

NENO LAONEKANA KATIKA MWILI

BIBLIA TAKATIFU
ENZI YA UFALME

Dibaji

Ingawa watu wengi wanaamini katika Mungu, ni wachache wanaoelewa ni nini maana ya imani katika Mungu, na ni nini wanachopaswa kufanya ili waupendeze moyo wa Mungu. Hii ni kwa sababu, hata ingawa watu wengi wanalifahamu neno “Mungu” na mafungu ya maneno kama “kazi ya Mungu”, hawamjui Mungu, sembuse kujua kazi ya Mungu. Si ajabu, basi, kwamba wale wote wasiomjua Mungu wamejawa na imani iliyovurugika. Watu hawachukulii imani kwa Mungu kwa uzito kwa kuwa kuamini Mungu ni jambo geni, jambo lisilo la kawaida sana kwao. Kwa njia hii, hawafikii mahitaji ya Mungu. Kwa maneno mengine, ikiwa watu hawamjui Mungu, hawajui kazi Yake, basi hawafai kwa matumizi na Mungu, sembuse kuweza kutimiza hamu ya Mungu. “Imani katika Mungu” inamaanisha kuamini kuwa kuna Mungu; hii ndiyo dhana rahisi zaidi ya imani katika Mungu. Zaidi ya hayo, kuamini kuwa kuna Mungu si sawa na kuamini katika Mungu kwa ukweli; bali, ni aina ya imani sahili ikiwa na vipengee vya uzito vya kidini. Imani ya kweli katika Mungu ina maana kupitia maneno na kazi ya Mungu kwa msingi wa imani kuwa Mungu ndiye mkuu juu ya vitu vyote. Kwa hivyo mtawekwa huru kutokana na tabia yenu ya upotovu, mtatimiza hamu ya Mungu, na mtapata kumjua Mungu. Ni kwa kupitia safari ya aina hii tu ndio mnaweza kusemekana kuwa mnaamini katika Mungu. Ilhali watu mara nyingi huona kuamini katika Mungu kama jambo rahisi sana na la kipuuzi tu. Watu wanaomwami Mungu kwa njia hii wamepoteza maana ya kumwamini Mungu, na ingawa wanaweza kuendelea kuamini mpaka mwisho, hawatawahi kupata idhini ya Mungu, kwa sababu wanatembea katika njia mbaya. Leo, kuna wale ambao bado wanaamini Mungu katika nyaraka, katika mafundisho ya dini yaliyo matupu. Hawana habari kuwa imani yao katika Mungu haina dutu, na hawawezi kupata idhini ya Mungu, na bado wanaomba kupata amani na neema ya kutosha kutoka kwa Mungu. Tunafaa kuweka kituo na kujiuliza wenyewe: Je, kuamini kwa Mungu linaweza kuwa jambo rahisi ya yote duniani? Je, kuamini kwa Mungu hakumaanishi chochote zaidi ya kupokea neema nyingi kutoka kwa Mungu? Je, watu wanaoamini kwa Mungu na hawamjui, na wanaamini kwa Mungu ila wanamuasi; je watu kama hawa wanaweza kutimiza hamu ya Mungu?

Mungu na mwanadamu hawawezi kuzungumziwa kama wa kulingana. Dutu ya Mungu na kazi Yake ni vitu visivyoeleweka na kufahamika kwa mwanadamu. Ikiwa Mungu hawezi kufanya kazi Yake binafsi na kuzungumza maneno Yake katika ulimwengu wa mwanadamu, basi mwanadamu hangeweza kuelewa mapenzi ya Mungu, na kwa hivyo, hata wale waliotoa maisha yao yote kwa ajili ya Mungu hawataweza kupata idhini ya Mungu. Bila kazi ya Mungu, haijalishi jinsi gani mwanadamu anatenda mema, haitahesabika kama chochote, kwa maana fikira za Mungu daima zitakuwa juu ya fikira za mwanadamu, na hekima ya Mungu haieleweki kwa mwanadamu. Na kwa hivyo Nasema kwamba wale ambao “wanaona kwa wazi”. Mungu na

kazi Yake ni wasioweza kufanikisha chochote, wao wote ni wenye kiburi na wapumbavu. Mwanadamu hafai kufafanua kazi ya Mungu; zaidi ya hayo, mwanadamu hawezi kufafanua kazi ya Mungu. Katika macho ya Mungu, mwanadamu ni mdogo kushinda mchwa, kwa hivyo mwanadamu atawezaje kuelewa kazi ya Mungu? Wale wasemao daima, “Mungu hafanyi kazi kwa njia hii ama ile” au “Mungu yuko hivi ama vile”—je hawa wote si wenye kiburi? Tunafaa sote kujua kwamba watu, ambao ni wa mwili, wote wamepotoshwa na Shetani. Ni katika hali yao asili kumuasi Mungu, na hawako katika usawa na Mungu, sembuse kuweza kutoa mawaidha kwa kazi ya Mungu. Jinsi Mungu anavyomwelekeza mwanadamu ni kazi ya Mungu mwenyewe. Mwanadamu anafaa kunyenyekea, na hafai kuwa na wazo hili ama lile, kwani mwanadamu ni mchanga tu. Kwa sababu tunajaribu kumtafuta Mungu, hatufai kuwekelea dhana zetu katika kazi ya Mungu ili Mungu Aziwaze, na zaidi hatufai kutumia tabia zetu potovu kwa kupinga kazi ya Mungu kwa makusudi. Je hili halitatumia wapinga Kristo? Je, watu kama hawa watawezaje kusema kuwa wanamwamini Mungu? Kwa maana tunaamini kuwa kuna Mungu, na kwa maana tunatamani kumtosheleza na kumwona, tunapaswa kutafuta njia ya ukweli, na tunapaswa kutafuta njia ya kulingana na Mungu. Hatupaswi kuwa katika upinzani sugu kwa Mungu; Matendo kama haya yatakuwa na matokeo gani mazuri?

Leo hii, Mungu Anayo kazi mpya. Unaweza kuyakataa maneno haya, yanaweza kuhisi yasiyo ya kawaida kwako, lakini Nakushauri usifichue asili yako halisi, kwa maana wale tu walio na njaa ya kweli na kiu cha haki mbele za Mungu ndio wanaweza kupata ukweli, na wale wanaomcha Mungu kwa ukweli tu ndio wanaweza kupata nuru na kuongozwa na Mungu. Hakuna litakalotoka kwa kutafuta ukweli kupitia ugomvi. Ni kwa kutafuta kwa utulivu ndio tunaweza kupata matokeo. Ninaposema kwamba “leo, Mungu Anayo kazi mpya,” Ninaashiria Mungu kurudi katika mwili. Pengine huyajali maneno haya, pengine unayachukia, au pengine una haja kubwa sana nayo. Haijalishi ni hali gani, Natumai kuwa wote walio na tamaa ya kweli ya kuonekana kwa Mungu wataweza kuukabili ukweli huu na kutafakari juu yake kwa makini. Ni vyema usiamue jambo upesi bila kuzingatia suala zima. Hivi ndivyo watu wenye hekima wanapaswa kutenda.

Kuchunguza kitu cha aina hii sio vigumu, lakini kunahitaji kila mmoja wetu ajue ukweli huu: Yeye Aliye mwili wa Mungu Atakuwa na dutu ya Mungu, na Yule Aliye Mungu katika mwili Atakuwa na maonyesho ya Mungu. Kwa maana Mungu Hupata mwili, Ataleta mbele kazi Anayopaswa kufanya, na kwa maana Mungu Amapata mwili, Ataonyesha kile Alichoko na Ataweza kuuleta ukweli kwa mwanadamu, kumpa mwanadamu uhai, na Amwonyeshe mwanadamu njia. Mwili usio na dutu ya Mungu kwa kweli sio Mungu mwenye mwili; kwa hili hakuna tashwishi. Kupeleleza kama kweli ni mwili wa Mungu mwenye Mwili, mwanadamu lazima aamue haya kutoka kwa tabia Yeye huonyesha na maneno Yeye hunena. Ambayo ni

kusema, kama ni mwili wa Mungu mwenye mwili au la, na kama ni njia ya kweli au la, lazima iamuliwe kutokana na dutu Yake. Hivyo, katika kudadisi^[a] iwapo ni mwili wa Mungu mwenye mwili, cha msingi ni kuwa makini kuhusu dutu Yake (Kazi Yake, maneno Yake, tabia Yake, na mengine mengi), bali sio hali ya sura Yake ya nje. Mwanadamu akiona tu sura Yake ya nje, na aipuuze dutu Yake, basi hilo linaonyesha upumbavu na ujinga wa mwanadamu. Sura ya nje haiamulii dutu; na zaidi, kazi ya Mungu haiwezi kamwei kuambatana na dhana za mwanadamu. Je, si sura ya nje ya Yesu ilikinzana na dhana za mwanadamu? Je sura Yake na mavazi Yake hayakuweza kutoa dalili yoyote ya utambulisho Wake? Je, si sababu ya Mafarisayo wa zamani kabisa kumpinga Yesu hasa ilikuwa ni kwa sababu waliangalia tu sura Yake ya nje, na hawakuyaweka moyoni maneno Aliyoongea? Ni matumaini Yangu kuwa ndugu wanaotafuta kuonekana kwa Mungu hawatarudia tanzia ya kihistoria. Hampaswi kuwa Mafarisayo wa wakati huu na kumsulubisha Mungu msalabani tena. Mnafaa kufikiria kwa makini jinsi ya kukaribisha kurudi kwa Mungu, na kuwa na mawazo dhahiri ya jinsi ya kuwa mtu anayetii ukweli. Hili ni jukumu la kila mtu anayengoja Yesu arudi na mawingu. Tunafaa kusugua macho yetu ya kiroho, na tusiwe waathiriwa wa maneno yaliyojaa mambo ya kufurahisha masikio. Tunafaa kuwaza juu ya kazi ya Mungu ya matendo, na tunafaa kuangalia upande wa hakika wa Mungu. Msijisahau ama kupotelea ndotoni, mkitazamia daima ile siku ambayo Bwana Yesu atashuka kwa ghafla juu ya mawingu kuwachukua nyinyi ambao hamjawahi kumjua wala kumwona Yeye, na msiojua kutenda mapenzi Yake. Ni vyema kufikiri juu ya mambo ya kiutendaji!

Unaweza kuwa umefungua kitabu hiki kwa ajili ya utafiti, au ukiwa na nia ya kukubali; haijalishi mwelekeo wako, Natumaini kuwa utakisoma mpaka mwisho, na hutakiweka kando kwa urahisi. Pengine, baada ya kuyasoma maneno haya, mwelekeo wako utabadilika, lakini hilo linategemea na motisha yako na kiwango chako cha ufahamu. Kunalo jambo moja hata hivyo unalotakiwa kujua: Neno la Mungu haliwezi kuzungumzwa kama neno la mwanadamu, sembuse neno la mwanadamu kuzungumzwa kama neno la Mungu. Mwanadamu anayetumiwa na Mungu siye Mungu mwenye mwili, na Mungu mwenye mwili siye mwanadamu anayetumiwa na Mungu; katika hili, kunayo tofauti kubwa sana. Pengine, baada ya kusoma maneno haya, hukubali kuwa ni maneno ya Mungu, na kuyakubali tu kama maneno ya mwanadamu ambaye amepewa nuru. Ikiwa hivyo, basi umepofushwa na ujinga. Maneno ya Mungu yatawezaje kuwa sawa na maneno ya mwanadamu ambaye amepewa nuru? Maneno ya Mungu mwenye mwili yanaanzisha enzi mpya, yanaongoza wanadamu wote, yanafichua mafumbo, na kumwonyesha mwanadamu mwelekeo mbele katika enzi mpya. Nuru anayoipata mwanadamu ni utendaji au elimu rahisi. Haiwezi kuelekeza binadamu wote kuingia enzi mpya au kufichua fumbo la Mungu Mwenyewe. Mungu, hata hivyo, ni Mungu, na mwanadamu ni mwanadamu. Mungu yuko na dutu ya Mungu, na mwanadamu yuko na dutu ya mwanadamu. Iwapo mwanadamu anachukulia

maneno yanayonenwa na Mungu kama kupewa nuru tu na Roho Mtakatifu, na kuchukua maneno yaliyonenwa na mitume na manabii kama maneno yaliyonenwa na Mungu Mwenyewe, basi mwanadamu anakosea. Licha ya haya, hufai kamwe kubadili jambo sahihi liwe baya, ama kuzungumzia lililo juu kama la chini, au kuzungumzia jambo kubwa kama lisilo na kina; haijalishi ni nini, hupaswi kamwe kwa makusudi kupinga lile unalojua kuwa ni ukweli. Kila anayeamini kuwa kuna Mungu anapaswa kufikiri juu ya tatizo hili kwa msimamo ulio sahihi, na anapaswa kukubali kazi Yake mpya na maneno Yake kama kiumbe wa Mungu—la sivyo aondolewe na Mungu.

Baada ya kazi ya Yehova, Yesu Alipata mwili ili Afanye kazi Yake miongoni mwa wanadamu. Kazi Yake haikutekelezwa kivyake, ila ilijengwa juu ya misingi ya kazi ya Yehova. Ilikuwa kazi ya enzi mpya baada ya Mungu kukamilisha Enzi ya Sheria. Vivyo hivyo, baada ya kazi ya Yesu kukamilika, Mungu bado Aliendeleza kazi Yake ya enzi iliyofuata, kwa sababu usimamizi wote wa Mungu huendelea mbele siku zote. Enzi nzee ikipita, itabadilishwa na enzi mpya, na mara tu kazi nzee imekamilika, kazi mpya itaendeleza usimamizi wa Mungu. Kupata mwili huku ni kupata mwili kwa Mungu mara ya pili kufuatia kukamilika kwa kazi ya Yesu. Bila shaka, kupata mwili huku hakufanyiki kivyake, bali ni hatua ya tatu ya kazi baada ya Enzi ya Sheria na Enzi ya Neema. Kila hatua mpya ya kazi ya Mungu kila mara huleta mwanzo mpya na enzi mpya. Vivyo hivyo kuna mabadiliko yanayokubaliana katika tabia ya Mungu, katika njia Yake ya kufanya kazi, katika sehemu Yake ya kufanya kazi, na katika jina Lake. Ndiyo maana basi ni vigumu kwa mwanadamu kukubali kazi ya Mungu katika enzi mpya. Lakini licha ya jinsi anapingwa na mwanadamu, Mungu huendelea kufanya kazi Yake, na daima Yeye huwa Akiongoza wanadamu wote kuendelea mbele. Yesu Alipokuja katika ulimwengu wa mwanadamu, Alileta Enzi ya Neema na Akatamatisha Enzi ya Sheria. Wakati wa siku za mwisho, Mungu kwa mara nyingine Alipata mwili, na Alipopata mwili mara hii, Alikamilisha Enzi ya Neema na Akaleta Enzi ya Ufalme. Wale wote wanaokubali kupata mwili kwa Mungu kwa mara ya pili wataongozwa mpaka Enzi ya Ufalme, na wataweza kukubali kibinafsi uongozi wa Mungu. Hata ingawa Yesu Alifanya kazi nyingi miongoni mwa wanadamu, Yeye Alimaliza tu ukombozi wa wanadamu wote na akawa sadaka ya dhambi ya mwanadamu, na Hakumwondolea mwanadamu tabia yake yote ya upotovu. Kumwokoza mwanadamu kikamilifu kutokana na ushawishi wa Shetani hakukumlazimu Yesu kuchukua dhambi zote za mwanadamu kama sadaka ya dhambi tu, lakini pia kulimlazimu Mungu kufanya kazi kubwa zaidi ili kumwondolea mwanadamu tabia yake kikamilifu, ambayo imepotoshwa na Shetani. Na kwa hivyo, baada ya mwanadamu kusamehewa dhambi zake, Mungu Amerudi katika mwili kumwongoza mwanadamu katika enzi mpya, na kuanza kazi ya kuadibu na hukumu, na kazi hii imemleta mwanadamu katika ulimwengu wa juu zaidi. Wote wanaonyenyekea chini ya utawala

Wake watapata kufurahia ukweli wa juu na kupata baraka nyingi mno. Wataishi katika mwanga kwa kweli, na watapata ukweli, njia na uzima.

Watu wakibaki katika Enzi ya Neema, basi hawatawahi kujiweka huru kutokana na tabia zao za upotovu, sembuse kujua tabia ya asili ya Mungu. Wanadamu wakiishi daima katika wingi wa neema ila hawana njia ya maisha inayowaruhusu kumjua Mungu na kumridhisha Mungu, basi kamwe hawataweza kumpata Mungu kwa kweli hata ingawa wanaamini Kwake. Hiyo ni aina ya imani ya kutia huruma. Wakati umemaliza kusoma kitabu hiki, wakati umepitia matukio yote ya kazi ya Mungu mwenye mwili katika Enzi ya Ufalme, utahisi kwamba matumaini ya miaka mingi hatimaye yametimika. Utahisi kwamba ni sasa tu ndipo umemwona Mungu uso kwa uso; ni sasa tu ndipo umeutazama uso wa Mungu, umesikia matamshi ya Mungu Mwenyewe, umeifahamu hekima ya kazi ya Mungu, na kuhisi kwa kweli jinsi Mungu ni wa kweli na mwenye nguvu. Utafahamu kuwa umepata vitu vingi ambavyo watu wa nyakati zilizopita hawajawahi kuviona wala kuwa navyo. Wakati huu, utajua kwa uhakika ni nini hasa kuamini katika Mungu, na ni nini kupendeza nafsi ya Mungu. Bila shaka, ukikwamilia maoni ya kitambo, na ukatae au ukane ukweli wa kupata mwili kwa Mungu mara ya pili, basi utabaki mkono mtupu na hutapata chochote, na mwishowe utakuwa na hatia ya kumpinga Mungu. Wale wanaotii ukweli na kunyenyekea kwa kazi ya Mungu watakuja chini ya jina la Mungu mwenye mwili wa pili—Mwenyezi. Wataweza kukubali uelekezi binafsi wa Mungu, na watapata ukweli zaidi na wa juu zaidi na watapokea maisha ya kweli ya mwanadamu. Wataona maono ambayo watu wa zamani hawajawahi kuona kamwe: “Na nikapinduka ili kuiona sauti hiyo iliyonizungumzia. Na baada ya kupinduka, nikatazama vinara saba vya taa vilivyokuwa vya dhahabu; Na hapo katikati ya hivyo vinara saba vya taa nilimwona mtu aliyefanana na Mwana wa Adamu, aliyekuwa amevalia nguo iliyofika katika miguu yake, na kifuni alikuwa amefungwa kanda ya dhahabu. Kichwa chake na nywele zilikuwa nyeupe mithili ya sufu, nyeupe mithili ya theluji; na macho yake yalikuwa mithili ya ulimi wa moto; Na miguu yake mithili ya shaba safi, kama kwamba ilikuwa imechomwa ndani ya tanuru; na sauti yake ilikuwa mithili ya sauti ya maji mengi. Na katika mkono wake wa kulia kulikuwa na nyota saba: na alitoa kinywani mwake upanga mkali wenye sehemu mbili za makali: nao uso wake ulikuwa mithili ya jua liangazavyo kupitia nguvu zake yeye” (Ufunuo 1:12-16). Maono haya ni maonyesho ya tabia kamilifu ya Mungu, na maonyesho ya aina hii ya tabia Yake nzima pia ndiyo maonyesho ya kazi ya Mungu Anapopata mwili mara hii. Katika mibubujiko ya kuadibu na hukumu, Mwana wa Adamu Anaonyesha tabia Yake ya asili kupitia kuzungumza kwa maneno, Akiwaruhusu wale wote wanaokubali kuadibu Kwake na hukumu kuuona uso wa kweli wa Mwana wa Adamu, uso ulio mfano wa kuaminika wa Mwana wa Adamu Alivyooneka na Yohana. (Bila shaka, yote haya hayatawaonekana wote wasioikubali kazi ya Mungu katika Enzi ya Ufalme.) Uso wa kweli wa

Mungu hauwezi kuelezwa kikamilifu na maneno ya mwanadamu, na hivyo Mungu Hutumia maonyesho ya tabia Yake asili kuuonyesha uso Wake wa kweli kwa mwanadamu. Ambayo ni kusema wote ambao wamepitia tabia asili ya Mwana wa Adamu wameuona uso wa kweli wa Mwana wa Adamu, kwa kuwa Mungu ni mkuu zaidi na Hawezi kuelezwa kikamilifu na maneno ya mwanadamu. Mara tu mwanadamu amepitia kila hatua ya kazi ya Mungu katika Enzi ya Ufalme, basi atapata kujua maana kamili ya maneno ya Yohana alipozungumza kuhusu Mwana wa Adamu kati ya vinara vya taa: “Kichwa chake na nywele zilikuwa nyeupe mithili ya sufu, nyeupe mithili ya theluji; na macho yake yalikuwa mithili ya ulimi wa moto; Na miguu yake mithili ya shaba safi, kama kwamba ilikuwa imechomwa ndani ya tanuru; na sauti yake ilikuwa mithili ya sauti ya maji mengi. Na katika mkono wake wa kulia kulikuwa na nyota saba: na alitoa kinywani mwake upanga mkali wenye sehemu mbili za makali: nao uso wake ulikuwa mithili ya jua liangazavyo kupitia nguvu zake yeye.” Wakati huo, utajua bila shaka yoyote kwamba mwili huu wa kawaida uliozungumza maneno mengi ni kwa hakika Mungu mwenye mwili mara ya pili. Na utahisi ni jinsi gani kwa kweli umebarikiwa, na kujiona mwenyewe kama mwenye bahati kubwa. Je, ungekuwa huna radhi kuikubali baraka hii?

Sehemu ya kwanza ya kitabu hiki ni “Matamshi ya Kristo Mwanzoni”. Maneno haya yanawakilisha mpito kutoka mwisho wa Enzi ya Neema hadi kwa mwanzo wa Enzi ya Ufalme, na ni ushuhuda wa wazi wa Roho Mtakatifu wa Mwana wa Adamu kwa makanisa. Pia ni utimizo wa maneno katika Ufunuo wa Yohana kwamba “Yeye ambaye ana sikio, na asikie yale ambayo makanisa yaliambiwa na Roho.” Hii ni kazi ambayo Mungu alianza katika Enzi ya Ufalme. Sehemu ya pili ya kitabu hiki ni maneno ambayo yaliyonenwa binafsi na Mwana wa Adamu baada ya Yeye kujifichua kirasmi. Inajumuisha maudhui kubwa ya matamshi kadhaa tofauti na maneno kama vile unabii, ufunuo wa mafumbo, na njia ya maisha. Kuna utabiri wa siku za usoni ya ufalme, ufunuo wa mafumbo ya mpango wa usimamizi wa Mungu, uchunguzi wa asili ya mwanadamu, ushawishi na maonyo, hukumu kali, maneno ya dhati ya kuliwaza, mazungumzo ya maisha, mazungumzo ya kuingia na kadhalika. Kwa ufupi, kile Mungu Anacho na Alichu, na tabia ya Mungu yote imeonyeshwa ndani ya kazi na maneno Yake. Bila shaka, Mungu Anapopata mwili mara hii, kazi Yake ni kuonyesha tabia Yake, kimsingi kupitia kuadibu na hukumu. Akitumia haya kama msingi, Analeta ukweli zaidi kwa mwanadamu, kuonyesha njia zaidi za matendo, na hivyo Hufikia lengo Lake la kumshinda mwanadamu na kumwokoza mwanadamu kutokana na tabia yake potovu. Hili ndilo liko katika kazi ya Mungu katika Enzi ya Ufalme. Je, unatamani kuingia katika enzi mpya? Je, unatamani kujiondolea tabia yako potovu? Je, unatamani kupata ukweli wa juu? Je, unatamani kuuona uso wa kweli wa Mwana wa Adamu? Je unatamani kuishi maisha yaliyo na thamani? Je, unatamani kufanywa mkamilifu na Mungu? Basi, je, utakaribisha vipi kurudi kwa Yesu?

Tanbihi:

a. Nakala halisi ya mwanzo inasema “na kwa.”

Yaliyomo

**Sehemu ya Kwanza Matamko ya Kristo Mwanzoni —Maneno ya Roho Mtakatifu kwa
Makanisa (Februari 11, 1991 hadi Novemba 20, 1991)**

Utangulizi

Sura ya 1

Sura ya 2

Sura ya 3

Sura ya 4

Sura ya 5

Sura ya 6

Sura ya 7

Sura ya 8

Sura ya 9

Sura ya 10

Sura ya 11

Sura ya 12

Sura ya 13

Sura ya 14

Sura ya 15

Sura ya 16

Sura ya 17

Sura ya 18

Sura ya 19

Sura ya 20

Sura ya 21

Sura ya 22

Sura ya 23

Sura ya 24

Sura ya 25

Sura ya 26

Sura ya 27
Sura ya 28
Sura ya 29
Sura ya 30
Sura ya 31
Sura ya 32
Sura ya 33
Sura ya 34
Sura ya 35
Sura ya 36
Sura ya 37
Sura ya 38
Sura ya 39
Sura ya 40
Sura ya 41
Sura ya 42
Sura ya 43
Sura ya 44
Sura ya 45
Sura ya 46
Sura ya 47
Sura ya 48
Sura ya 49
Sura ya 50
Sura ya 51
Sura ya 52
Sura ya 53
Sura ya 54
Sura ya 55
Sura ya 56
Sura ya 57
Sura ya 58
Sura ya 59
Sura ya 60
Sura ya 61
Sura ya 62

Sura ya 63
Sura ya 64
Sura ya 65
Sura ya 66
Sura ya 67
Sura ya 68
Sura ya 69
Sura ya 70
Sura ya 71
Sura ya 72
Sura ya 73
Sura ya 74
Sura ya 75
Sura ya 76
Sura ya 77
Sura ya 78
Sura ya 79
Sura ya 80
Sura ya 81
Sura ya 82
Sura ya 83
Sura ya 84
Sura ya 85
Sura ya 86
Sura ya 87
Sura ya 88
Sura ya 89
Sura ya 90
Sura ya 91
Sura ya 92
Sura ya 93
Sura ya 94
Sura ya 95
Sura ya 96
Sura ya 97
Sura ya 98

Sura ya 99
Sura ya 100
Sura ya 101
Sura ya 102
Sura ya 103
Sura ya 104
Sura ya 105
Sura ya 106
Sura ya 107
Sura ya 108
Sura ya 109
Sura ya 110
Sura ya 111
Sura ya 112
Sura ya 113
Sura ya 114
Sura ya 115
Sura ya 116
Sura ya 117
Sura ya 118
Sura ya 119
Sura ya 120

Sehemu ya Pili Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima (Februari 20, 1992 hadi Juni 1, 1992)

Utangulizi
Sura ya 1
Sura ya 2
Sura ya 3
Sura ya 4
Sura ya 5
Sura ya 6
Sura ya 7
Sura ya 8
Sura ya 9
Sura ya 10

Wimbo wa Ufalme

Sura ya 11

Sura ya 12

Sura ya 13

Sura ya 14

Sura ya 15

Sura ya 16

Sura ya 17

Sura ya 18

Sura ya 19

Sura ya 20

Sura ya 21

Sura ya 22

Sura ya 23

Sura ya 24

Sura ya 25

Furahini, Enyi Watu Wote!

Sura ya 26

Sura ya 27

Sura ya 28

Sura ya 29

Sura ya 30

Sura ya 31

Sura ya 32

Sura ya 33

Sura ya 34

Sura ya 35

Sura ya 36

Sura ya 37

Sura ya 38

Sura ya 39

Sura ya 40

Sura ya 41

Sura ya 42

Sura ya 43

Sura ya 44

Sura ya 45

Sura ya 46

Sura ya 47

Kiambatisho: Ufafanuzi wa Mafumbo ya Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima (Ufafanuzi wa Baadhi ya Sura)

Sura ya 1

Sura ya 3

Sura ya 4

Sura ya 5

Sura ya 6

Kuhusu Maisha ya Petro

Sura ya 8

Sura ya 9

Nyongeza: Sura ya 1

Sura ya 10

Sura ya 11

Nyongeza: Sura ya 2

Sura ya 12

Sura ya 13

Sura ya 14

Sura ya 15

Sura ya 16

Sura ya 17

Sura ya 18

Sura ya 19

Sura ya 20

Sura ya 21

Sura ya 22 na 23

Sura ya 24 na 25

Sura ya 26

Sura ya 27

Sura ya 28

Sura ya 29

Sura ya 30

Sura ya 31

Sura ya 32

Sura ya 33
Sura ya 35
Sura ya 36
Sura ya 38
Sura ya 39
Sura ya 40
Sura ya 41
Sura ya 42
Sura ya 44 na 45
Sura ya 46

Sehemu ya Tatu Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani (Juni 1992 hadi Agosti 2014)

Utangulizi

Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani I (Juni 1992 hadi Oktoba 1992)

Njia ... (1)
Njia ... (2)
Njia ... (3)
Njia ... (4)
Njia ... (5)
Njia ... (6)
Njia ... (7)
Njia ... (8)

Maoni Wanayopaswa Kushikilia Waumini

Kwenye Hatua za Kazi ya Mungu

Mwanadamu Mpotovu Hawezi Kumwakilisha Mungu

Njia ya Huduma ya Kidini Lazima Ipigwe Marufuku

Katika Imani Yako kwa Mungu Unapaswa Kumtii Mungu

Ni Muhimu Sana Kuanzisha Uhusiano wa Kawaida na Mungu

Maisha Ya Kawaida ya Kiroho Huwaongoza Watu Kwenye Njia Sahihi

Ahadi kwa Wale Ambao Wamekamilishwa

Waovu Hakika Wataadhibiwa

Jinsi ya Kuingia Katika Hali ya Kawaida

Jinsi ya Kuhudumu kwa Upatanifu na Mapenzi ya Mungu

Jinsi ya Kujua Uhalisi

Kuhusu Maisha ya Kawaida ya Kiroho
Kujadili Maisha ya Kanisa na Maisha Halisi
Kuhusu Kila Mmoja Kutekeleza Wajibu Wake
Kuhusu Mungu Kumtumia Mwanadamu
Punde Unapoelewa Ukweli, Unapaswa Kuuweka Katika Vitendo
Mtu Anayepata Wokovu ni Yule Ambaye Yuko Tayari Kutenda Ukweli
Kile Ambacho Mchungaji wa Kutosha Anapaswa Kujiandaa Nacho
Kuhusu Uzoefu
Amri za Enzi Mpya
Ufalme wa Milenia Umewasili
Uhusiano Wako na Mungu Ukoje?
Sisitiza Uhalisi Zaidi
Kuzishika Amri na Kuutenda Ukweli
Unapaswa Kujua kuwa Mungu wa Vitendo Ni Mungu Mwenyewe
Kuuweka tu Ukweli Katika Matendo Ndiko Kuwa na Uhalisi
Kujua Kazi ya Mungu Leo
Je, Kazi ya Mungu Ni Rahisi Kama Vile Mwanadamu Anavyodhania?
Unapaswa Kuishi kwa Ajili ya Ukweli kwa Maana Unamwamini Mungu
Ngurumo Saba Zatoa Sauti—Zikitabiri Kuwa Injili ya Ufalme Itaenea Kote Ulimwenguni
Tofauti Muhimu Kati ya Mungu Mwenye Mwili na Watu Wanaotumiwa na Mungu
Epuka Ushawishi wa Giza na Utapatwa na Mungu
Katika Imani, Mtu Lazima Alenge Ukweli—Kujihusisha na Kaida za Dini Sio Imani
Ni Wale tu Wanaojua Kazi ya Mungu Leo Ndio Wanaoweza Kumhudumia Mungu
Upendo Halisi kwa Mungu ni wa Hiari
Kuhusu Desturi ya Sala
Jua Kazi Mpya Zaidi ya Mungu na Ufuate Nyayo Zake
Wale Ambao Tabia Zao Imabadilika ni Wale Ambao Wameingia Katika Uhalisi wa Neno la Mungu
Kuhusu Kuutuliza Moyo Wako Mbele ya Mungu
Kuwa Mzingatifu wa Mapenzi ya Mungu ili Upate Utimilifu
Mungu Anawakamilisha Wale Wanaoupendeza Moyo Wake
Wale Wanaomtii Mungu kwa Moyo wa Kweli Hakika Watapatwa na Mungu
Enzi ya Ufalme Ni Enzi ya Neno
Yote Yanafanikishwa Kupitia kwa Neno la Mungu
Wale Wanaompenda Mungu Kwa Kweli Ni Wale Wanaoweza Kutii Utendaji Wake Kabisa
Wale Wanaopaswa Kukamilishwa Lazima Wapitie Usafishaji

Ni kwa Kupitia tu Majaribio ya Kuumiza Ndiyo Mnaweza Kujua Kupendeza kwa Mungu
Kumpenda Mungu tu Ndiko Kumwamini Mungu Kweli
Mazungumzo Mafupi Kuhusu “Ufalme wa Milenia Umefika”
Wale Wanaomjua Mungu Pekee Ndio Wanaoweza Kuwa na Ushuhuda Kwa Mungu
Namna Petro Alivyopata Kumjua Yesu
Ni kwa Kupitia Usafishaji tu Ndiyo Mwanadamu Anaweza Kuwa na Upendo wa Kweli
Wanaompenda Mungu Wataishi Milele Katika Mwangaza Wake
Ni Wale Wanaolenga Kutenda tu Ndio Wanaoweza Kukamilishwa
Kazi ya Roho Mtakatifu na Kazi ya Shetani
Onyo kwa Wale Wasiotenda Ukweli
Unapaswa Kudumisha Ibada Yako kwa Mungu
Je, Wewe ni Mtu Ambaye Amepata Uzima?
Kuwa na Tabia Isiyobadilika Ni Kuwa katika Uadui na Mungu
Watu Wote Wasiomjua Mungu Ni Watu Wanaompinga Mungu

Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani II (Novemba 1992 hadi Juni 1993)

Kazi na Kuingia (1)
Kazi na Kuingia (2)
Kazi na Kuingia (3)
Kazi na Kuingia (4)
Kazi na Kuingia (5)
Kazi na Kuingia (6)
Kazi na Kuingia (7)
Kazi na Kuingia (8)
Kazi na Kuingia (9)
Kazi na Kuingia (10)
Maono ya Kazi ya Mungu (1)
Maono ya Kazi ya Mungu (2)
Maono ya Kazi ya Mungu (3)
Kuhusu Biblia (1)
Kuhusu Biblia (2)
Kuhusu Biblia (3)
Kuhusu Biblia (4)
Utendaji (1)
Utendaji (2)
Fumbo la Kupata Mwili (1)

Fumbo la Kupata Mwili (2)
Fumbo la Kupata Mwili (3)
Fumbo la Kupata Mwili (4)
Kupata Mwili Mara Mbili Kunakamilisha Umuhimu wa Kupata Mwili
Je, Utatu Upo?
Utendaji (3)
Utendaji (4)
Utendaji (5)
Ukweli wa Ndani wa Kazi ya Ushindi (1)
Mbona Huna Hiari ya Kuwa Foili?
Jinsi Athari za Hatua ya Pili ya Kazi ya Ushindi Zinavyotimizwa
Ukweli wa Ndani wa Kazi ya Ushindi (2)
Ukweli wa Ndani wa Kazi ya Ushindi (3)
Ukweli wa Ndani wa Kazi ya Ushindi (4)
Utendaji (6)
Utendaji (7)
Utendaji (8)
Hudumu Jinsi Waisraeli Walivyohudumu
Kuboresha Ubora wa Tabia ni Kwa Ajili ya Kupokea Wokovu wa Mungu
Umuhimu wa Kuukoa Uzao wa Moabu
Matukio Aliyopitia Petro: Ufahamu Wake wa Adabu na Hukumu
Ni Lazima Muielewe Kazi—Msifuate kwa Rabsha!
Jinsi Unavyopaswa Kuitembea Sehemu ya Mwisho ya Njia
Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani III (Julai 1993 hadi Machi 1994)
Unapaswa Kushughulikiaje Wito Wako wa Baadaye?
Kusudi la Kuwasimamia Binadamu
Asili na Utambulisho wa Mwanadamu
Utambulisho wa Asili wa Mwanadamu na Thamani Yake: Je, Viko Namna Gani?
Wale Wasiojifunza na Wanaosalia Wajinga: Je, Wao Sio Wanyama?
Watu Waliochaguliwa wa China Hawana Uwezo wa Kuwakilisha Kabila Lolote la Israeli
Ufahamu wako wa Baraka ni Upi?
Ufahamu Wako Kumhusu Mungu Ni Upi?
Maana ya Kuwa Mtu Halisi
Unajua Nini Kuhusu Imani?
Majani Yaangukayo Yatakaporudi kwa Mizizi Yake, Utajuta Maovu Yote Ambayo Umefanya
Hakuna Aliye wa Mwili Anayeweza Kuepuka Siku ya Ghadhabu

Mwokozi Amerudi Tayari Juu ya “Wingu Jeupe”
Kazi ya Kueneza Injili Ni Kazi ya Kuokoa Binadamu Pia
Ninyi Nyote Ni Waovu Sana Katika Tabia!
Kazi katika Enzi ya Sheria
Maelezo ya Kweli ya Kazi Katika Enzi ya Ukombozi
Maneno kwa Vijana na kwa Wazee
Unapaswa Kujua Namna Ambavyo Binadamu Wote Wameendelea Hadi Siku ya Leo
Kuhusu Majina na Utambulisho
Wale Waliokamilishwa Pekee Ndio Wanaoweza Kuishi Maisha Yenye Maana
Mnapaswa Kuweka Pembeni Baraka za Hadhi na Kuelewa Mapenzi ya Mungu ya Kumletea
Mwanadamu Wokovu
Ni Jinsi Gani Ambavyo Mwanadamu Ambaye Amemwekea Mungu Mipaka katika Fikiria Zake
Anaweza Kupokea Ufunuo wa Mungu?
Ni Wale tu Wanaomjua Mungu na Kazi Yake Ndio Wanaoweza Kumridhisha Mungu
Tofauti Kati ya Huduma ya Mungu Mwenye Mwili na Wajibu wa Mwanadamu
Mungu Ndiye Bwana wa Viumbe Vyote
Msimamo Wako Kuhusu Nyaraka Kumi na Tatu ni Upi?
Mafanikio au Kushindwa Kunategemea Njia Ambayo Mwanadamu Hutembea
Kazi ya Mungu na Kazi ya Mwanadamu
Kujua Hatua Tatu za Kazi ya Mungu Ndiyo Njia ya Kumjua Mungu
Mwanadamu Aliyepotoka Anahitaji Zaidi Wokovu wa Mungu Mwenye Mwili
Kiini cha Mwili Ulio na Mungu
Kazi ya Mungu na Utendaji wa Mwanadamu
Kiini Cha Kristo Ni Utiifu kwa Mapenzi ya Baba wa Mbinguni
Kurejesha Maisha ya Kawaida ya Mwanadamu na Kumpeleka Kwenye Hatima ya Ajabu
Mungu na Mwanadamu Wataingia Rahani Pamoja
Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani IV (1994 hadi 1997, 2003 hadi 2005)
Kufikia Utakapouona Mwili wa Kiroho wa Yesu, Mungu Atakuwa Ametengeneza Upya Mbingu
na Dunia
Wale Ambao Hawalingani na Kristo Hakika Ni Wapinzani wa Mungu
Wengi Wanaitwa, Lakini Wachache Wanachaguliwa
Unapaswa Kutafuta Njia ya Uwiano na Kristo
Je, Wewe Ni Muumini wa Kweli wa Mungu?
Kristo Hufanya Kazi ya Hukumu kwa Ukweli
Je, Ulikuwa Unajua? Mungu Amefanya Jambo Kubwa Miongoni Mwa Wanadamu
Ni Kristo wa Siku za Mwisho Pekee Ndiye Anayeweza Kumpa Mwanadamu Njia ya Uzima wa
Milele

Tayarisha Matendo Mema ya Kutosha kwa ajili ya Hatima Yako

Wewe U Mwaminifu kwa Nani?

Juu ya Hatima

Maonyo Matatu

Dhambi Zitamwelekeza Mwanadamu Jahanamu

Ni Muhimu Sana Kuelewa Tabia ya Mungu

Jinsi ya Kumjua Mungu Duniani

Tatizo Zito Sana: Usaliti (1)

Shida Kubwa Sana: Usaliti (2)

Amri Kumi za Utawala Ambazo Lazima Wateule wa Mungu katika Enzi ya Ufalme Wazitii

Mnapaswa Kuzingatia Matendo Yenu

Mungu Ndiye Chanzo cha Uhai wa Mwanadamu

Kutanafusi kwa Mwenye Uweza

Kuonekana kwa Mungu Kumeleta Enzi Mpya

Mungu Anaongoza Majaliwa ya Wanadamu Wote

Mwanadamu Anaweza tu Kuokolewa Katikati ya Usimamizi wa Mungu

Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani (Kiendelezo) (Oktoba 17, 2013 hadi Agosti 18, 2014)

Kumjua Mungu Ndiyo Njia ya Kumcha Mungu na Kuepuka Maovu

Namna ya Kujua Tabia ya Mungu na Matokeo Ambayo Kazi Yake Itafanikisha

Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe I

Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe II

Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe III

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee I

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee II

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee III

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee IV

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee V

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee VI

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee VII

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee VIII

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee IX

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee X

Kiambatisho: Kutazama Kuonekana kwa Mungu katika Hukumu na Kuadibu Kwake

Hitimisho

Sehemu ya Kwanza
Matamko ya Kristo Mwanzoni
—Maneno ya Roho Mtakatifu kwa Makanisa
(Februari 11, 1991 hadi Novemba 20, 1991)
Utangulizi

Mnamo Februari 11, mwaka wa 1991, Mungu alitoa tamko Lake la kwanza katika kanisa, na tamko hili lilikuwa na athari isiyo ya kawaida kwa kila mmoja wa watu walioishi katika mkondo wa Roho Mtakatifu wakati huo. Tamko hili lilitaja yafuatayo: “Makazi ya Mungu yameonekana” na “Mkuu wa ulimwengu, Kristo wa siku za mwisho—Yeye ni Jua linalong’aa.” Kwa maneno haya ya maana sana, watu hawa wote waliletwa katika ulimwengu mpya. Wale wote waliosoma tamko hili walihisi maelezo ya kazi mpya, kazi kuu ambayo Mungu alikuwa karibu kuianzisha. Lilikuwa ni tamko hili zuri, tamu, na lenye habari nyingi katika maelezo machache liliwaleta binadamu wote katika kazi mpya ya Mungu na katika enzi mpya, na ambalo liliweka msingi na kuanzisha kazi ya Mungu katika kupata mwili huku. Mtu anaweza kusema kwamba tamko ambalo Mungu alitoa wakati huu ni lile ambalo linaunganisha enzi; kwamba ni wakati wa kwanza tangu mwanzo wa Enzi ya Neema ambapo Mungu amezungumza wazi kwa jamii ya binadamu; zaidi, kwamba ni wakati wa kwanza ambapo Amezungumza baada ya kujificha kwa miaka elfu mbili; na, zaidi ya hayo, kwamba ni utangulizi, sehemu muhimu ya kuanzia, kwa ajili ya kazi ambayo Mungu yuko karibu kuanza kufanya katika Enzi ya Ufalme.

Mara ya kwanza Mungu alipotoa tamko, Alifanya hivyo kwa njia ya sifa kutoka kwa mtazamo wa nafsi ya tatu, kwa lugha ambayo mara moja ilikuwa ya sanaa na ya ustaarabu na wazi na ya nyumbani, na vile vile ruzuku ya maisha ambayo ilieleweka kwa urahisi na bila shida. Akiwa na hili, Alilichukua kundi hili dogo la watu, waliojua tu jinsi ya kufurahia neema Yake wakingoja kwa hamu kurudi kwa Bwana Yesu, na kuwaleta kwa kimya katika hatua nyingine ya kazi katika mpango wa Mungu wa usimamizi. Katika hali hizi, binadamu hawakujua, sembuse kuthubutu kufikiri, ni aina gani ya kazi Mungu angeifanya hatimaye, ama yale ambayo yangetokea mbeleni. Baadaye, Mungu aliendelea kutoa matamko zaidi ili kuwaleta binadamu katika enzi mpya hatua kwa hatua. La kushangaza, kila tamko la Mungu ni tofauti katika maudhui na aidha hutumia aina tofauti za sifa na njia za maonyesho. Matamko haya, yaliyo sawa kwa sauti lakini ya namna mbalimbali katika maudhui, yamejazwa kila wakati na hisia za Mungu za utunzaji na kujali, na karibu kila moja lina ruzuku za maisha na maudhui tofauti na vile vile maneno ya kukumbusha, kushawishi, na kufariji kutoka kwa Mungu hadi kwa mwanadamu.

Katika matamko haya, mafungu kama hili yanaonekana mara kwa mara: “Mungu mmoja wa kweli Amekuwa mwili, Yeye ndiye Mkuu wa ulimwengu Ambaye hutawala vitu vyote”; “Mfalme wa ushindi hukaa juu ya kiti Chake cha enzi cha utukufu”; “Yeye hushikilia ulimwengu mikononi Mwake”; na kadhalika. Ujumbe unawasilishwa katika mafungu haya, ama mtu anaweza kusema kwamba mafungu haya yanawasilisha ujumbe kwa jamii ya binadamu: Mungu tayari Amekuwa katika dunia ya binadamu, Mungu ataanzisha kazi kubwa hata zaidi, ufalme wa Mungu tayari umeshuka katika kundi fulani la watu, na Mungu tayari Amapata utukufu na kuwashinda maadui Wake wengi. Kila mwanadamu anaelewa kila tamko la Mungu. Wanadamu wote wanamsubiri Mungu ayape sauti maneno mengi mapya hata zaidi, kwa sababu kila wakati Mungu anaponena, Yeye huutikisa moyo wa binadamu hadi katika kiini chake, na zaidi Anatawala na kuruzuku sawa kila mwendo na kila hisia ya mwanadamu, ili kwamba binadamu waanze kuyategemea na, na zaidi kuyaheshimu maneno ya Mungu hata zaidi kuvutiwa na maneno ya Mungu.... Kwa njia hii, pasipo kujua, kimsingi watu wengi sana walikuwa wameisahau Biblia, na hata waliyasikiliza shingo upande mahubiri ya kale na maandishi ya watu wa kiroho, kwa sababu hawakuweza kupata msingi wowote wa maneno haya ya Mungu katika maandishi ya zamani, wala hawakuweza kugundua mahali popote kusudi la Mungu katika kutoa matamko haya. Kwa sababu hiyo, iliwapasa binadamu kukiri kwa kiasi gani zaidi kwamba matamko haya ni sauti ya Mungu ambayo hayajaonwa wala kusikika tangu mwanzo wa wakati, kwamba yako mbali ya uwezo wa mtu yeyote anayemwamini Mungu, na kwamba yanapita chochote kilichosemwa na mtu yeyote wa kiroho katika enzi za zamani au matamko ya Mungu ya zamani. Wakihimizwa na kila moja ya matamko haya, binadamu waliingia katika hali ya kuashiria wema wa kazi ya Roho Mtakatifu bila kujua, katika maisha kwa safu ya mbele ya enzi mpya. Wakihimizwa na maneno ya Mungu, binadamu, wakiwa wamejawa na matarajio, walionja utamu wa kuongozwa binafsi na maneno ya Mungu. Naamini muda huu mfupi kuwa wakati ambapo kila binadamu ataangalia nyuma kwa kumbukumbu ya kuvumilia, wakati ambapo kwa kweli kile ambacho binadamu walifurahia wakati huu hakikuwa zaidi ya hali ya kuashiria wema wa kazi ya Roho Mtakatifu, au mtu anaweza kukiita ladha tamu ya sukari ambayo inaifunika dawa iliyo chini yake. Hii ni kwa sababu, kutoka wakati huu na kuendelea, bado chini ya mwongozo wa maneno ya Mungu, bado katika hali ya kuashiria wema wa kazi ya Roho Mtakatifu, binadamu waliongozwa katika awamu nyingine ya maneno ya Mungu pasipo kujua, ambayo ilikuwa hatua ya kwanza iliyohemshwa na tamko la Mungu katika Enzi ya Ufalme—jaribio la watendaji huduma.

Maneno yaliyotamkwa kabla ya jaribio la watendaji huduma yalikuwa hasa kwa njia ya maagizo, ushawishi, lawama, na kufundisha nidhamu, na katika sehemu nyingine yalitumia mtindo mzee wa mawasiliano uliotumiwa katika Enzi ya Neema—kutumia “Wanangu” kwa

wale waliomfuata Mungu ili kufanya iwe rahisi kwa binadamu kumkaribia Mungu, au ili binadamu waweze kuchukulia uhusiano wao na Mungu kuwa wa karibu. Kwa njia hii, hukumu yoyote ambayo Mungu alitoa kwa kujiona, majivuno na tabia nyingine potovu za binadamu, mwanadamu angeweza kuishughulikia na kuikubali katika utambulisho wake wa “mwana,” bila kuwa na uhasama kwa matamko ya “Mungu Baba,” zaidi ya hayo ahadi ambayo “Mungu Baba” alitoa kwa “wana” Wake haikuwa ya shaka kamwe. Katika kipindi hiki, binadamu wote walifurahia uwepo ulio huru kutokana na taabu kama ule wa mtoto mchanga, na hili lilitimiza kusudi la Mungu, yaani, walipoingia katika utu uzima, Angeanza kutekeleza hukumu kwao. Hili pia liliweka msingi wa kazi ya kuihukumu jamii ya binadamu ambayo Mungu anaanzisha rasmi katika Enzi ya Ufalme. Kwa sababu kazi ya Mungu katika kupata mwili huku hasa ni kuihukumu na kuishinda jamii nzima ya binadamu, punde mwanadamu alipochukua msimamo thabiti, Mungu aliingia katika mtindo wa kazi Yake mara moja—katika kazi ambayo Anamhukumu mwanadamu na kumwadibu. Kwa uwazi, matamko yote kabla ya jaribio la watendaji huduma yalitolewa kwa ajili ya kupitia mageuzi, lengo la kweli likiwa tofauti na lile lilioonekana kuwa. Nia ya Mungu yenye hamu ilikuwa kwamba Aweze kuzindua rasmi kazi Yake katika Enzi ya Ufalme punde iwezekanavyo. Kwa vyovyote vile, Hakutaka kuendelea kuwabembeleza binadamu kuelekea mbele kwa kuwapa vidonge vya dawa iliyopakwa sukari; badala yake, Alikuwa na hamu ya kuuona uso wa kweli wa kila mwanadamu mbele ya kiti Chake cha hukumu, na hata Alitaka kuona kwa hamu zaidi mtazamo wa kweli ambao binadamu wote wangukuwa nao kumwelekea baada ya kupoteza neema Yake. Alitaka tu kuona matokeo, si mchakato. Lakini wakati huo, hakukuwa na mtu aliyeelewa nia ya Mungu yenye hamu, kwa sababu moyo wa binadamu ulishughulika tu na hatima yake na matarajio yake ya baadaye. Si ajabu kwamba mara kwa mara, hukumu ya Mungu ilikuwa imeelekezwa kwa jamii nzima ya binadamu. Ilikuwa tu wakati binadamu walipoanza kuishi maisha ya kawaida ya binadamu, chini ya mwongozo wa Mungu, ndipo mtazamo wa Mungu kwa binadamu ulipobadilika.

Mwaka wa 1991 haukuwa wa kawaida: hebu tuuite mwaka huu “mwaka wa ustawi.” Mungu alianzisha kazi mpya ya Enzi ya Ufalme na kuelekeza matamshi Yake kwa jamii yote ya binadamu. Wakati huo huo, binadamu walifurahia wema wa pekee na, hata zaidi, kupitia uchungu unaoifuata hukumu ya Mungu ya pekee kwa mwanadamu. Jamii ya binadamu iliujua utamu usiojulikana, hukumu na hali ya kutupwa isiyojulikana, kana kwamba ilikuwa imempata Mungu na tena kana kwamba ilikuwa imempoteza Mungu. Kuteseka katika umiliki na kuteseka katika ufukara—hisia hizi zinajulikana tu na wale wanaozipitia binafsi; hisia hizi ni kitu ambacho mwanadamu hana uwezo wala njia ya kueleza. Majeraha ya aina hii ni yale Mungu alimpa kila mtu kama aina ya uzoefu na mali isiyoshikika. Maudhui ya matamko ambayo Mungu aliyatoa katika mwaka huu kweli yamo katika sehemu mbili kuu: Ya kwanza ni sehemu ambapo

Mungu alishuka katika dunia ya wanadamu ili kuwaalika binadamu waje mbele ya kiti Chake cha enzi kama wageni; ya pili, sehemu ambapo baada ya binadamu kula na kunywa hadi wakashiba, walitumiwa na Mungu kama watendaji huduma. Bila shaka ni dhahiri kwamba sehemu ya kwanza ni matakwa ya binadamu yenye thamani zaidi na ari zaidi, hasa kwa kuwa tangu zamani wanadamu wamezoea kufanya kufurahia kila kitu cha Mungu kuwa lengo la imani yao Kwake. Hii ndiyo maana, punde Mungu alipoanza kuyapa sauti matamko Yake, binadamu wote walikuwa tayari kuingia katika ufalme nao walisubiri hapo ili Mungu awape thawabu tofauti. Katika hali hizi watu hawakulipa gharama ya kufaa kabisa kwa kubadilisha tabia zao, kutafuta kumridhisha Mungu, kuyafikiria mapenzi ya Mungu na kadhalika. Kwa mtazamo wa haraka wa juu juu, wanadamu walionekana kushughulika huku na kule siku zote huku wakijitumia na kumfanyia Mungu kazi, wakati kwa kweli walikuwa wakifanya hesabu, katika mahala pa siri zaidi pa vina vya mioyo yao, hatua ifuatayo wanayopaswa kuchukua ili wapate baraka au kutawala kama wafalme. Mtu anaweza kusema kwamba, wakati moyo wa mwanadamu ulipokuwa ukimfurahia Mungu, ulikuwa ukifanyia Mungu hila wakati huo huo. Katika hali hii binadamu hukutana na chuki na karaha ya Mungu yenye kina zaidi; tabia ya Mungu haivumilii binadamu yeyote kumdanganya au kumtumia. Lakini hekima ya Mungu haifikiki na mwanadamu yeyote. Ilikuwa katikati ya kuvumilia mateso haya yote ambapo Alinena sehemu ya kwanza ya matamko Yake. Hakuna mwanadamu anayeweza kuwaza kuhusu kiasi cha mateso ambayo Mungu alivumilia, na kiasi cha kujali na fikira Alivyotumia wakati huu. Lengo la sehemu ya kwanza ya haya matamko ni kufichua aina tofauti za ubaya ambao mwanadamu huonyesha anapokabiliwa na cheo na faida, na kufichua ulafi na kustahili dharau kwa mwanadamu. Hata ingawa, katika kusema, Mungu huyafuma maneno Yake kwa sauti ya kweli na yenye ari ya mama anayependa, ghadhabu iliyo ndani kabisa mwa moyo Wake huchoma kama jua la mchana, kana kwamba limeelekezwa dhidi ya adui Zake. Kwa hali yoyote ile, Mungu hataki kuzungumza kwa kundi la watu ambao wamepungukiwa na usawa wa kawaida wa jamii ya binadamu, na hivyo, wakati wowote Anapozungumza, Anaizuia ghadhabu iliyo ndani ya moyo Wake ilhali wakati huo huo Akijizuia ili kutoa maonyesho kwa tamko Lake. Zaidi ya hayo Anazungumza kwa jamii ya binadamu isiyo na ubinadamu wa kawaida, isiyo na mantiki, iliyo potovu kabisa, yenye ulafi uliogeuka na kuwa asili ya pili, na isiyotii na inayomwasi Mungu kabisa. Vina ambavyo jamii ya mwanadamu imeanguka na kadiri ya chuki na karaha ya Mungu kwa jamii ya mwanadamu inaweza kufikiriwa kwa urahisi; jambo gumu kwa jamii ya binadamu kufikiri ni maumivu waliyompa Mungu—ambayo hayawezi kuelezwa kwa maneno. Lakini ilikuwa katika usuli huu hasa—ambapo hakuna mtu aliweza kugundua jinsi moyo wa Mungu unavyoteseka, na aidha hakuna mtu aliyegundua jinsi jamii ya binadamu isivyo na busara na isivyorekebisha—kwamba kila mtu, bila aibu yoyote au haya hata kidogo, alilichukulia kuwa jambo la kawaida kwamba alikuwa na haki kama wana wa Mungu kupokea

thawabu zote ambazo Alikuwa amemtayarishia mwanadamu, hata kufikia kiwango cha kugombana, mtu yeyote asitake kubaki nyuma na wote wakiogopa sana kupoteza. Kufikia sasa unapaswa kujua ni nafasi ya aina gani ambayo watu walioishi wakati huo walimiliki machoni pa Mungu. Jamii ya wanadamu kama hii inawezaje kupata thawabu za Mungu? Lakini kile ambacho mwanadamu hupokea kutoka kwa Mungu ni hazina ya thamani sana nyakati zote, na kinyume chake kile ambacho Mungu hupokea kutoka kwa mwanadamu ni uchungu mkubwa kabisa. Tangu mwanzoni mwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu, hiki ndicho mwanadamu amepokea daima kutoka kwa Mungu na kile ambacho amempa Mungu daima kama malipo.

Ingawa Mungu alijawa na wasiwasi, Alipoiona jamii hii ya binadamu, iliyo potovu kabisa, Hakuwa na budi kuitupa ndani ya jahanamu ili iweze kusafishwa. Hii ni sehemu ya pili ya tamko la Mungu, ambapo Mungu aliwatumia binadamu kama watendaji huduma Wake. Katika sehemu hii, Mungu alibadilika kutoka kuwa mpole hadi kuwa mkali, na kutoka machache hadi mengi, kuhusu mbinu na urefu, Akitumia nafasi ya “nafsi ya Mungu” kama ubembe ili kuifichua asili potovu ya mwanadamu na wakati huo huo Akiviweka mbele vikundi tofauti vya^[a] watendaji huduma, watu, na wana kwa watu ambao wangeweza kuchagua. Bila shaka, kama vile Mungu alivyokuwa Ametabiri, hakuna mtu aliyechagua kuwa mtendaji huduma kwa ajili ya Mungu, na badala yake wote walijitahidi kuwa nafsi ya Mungu. Hata ingawa, katika kipindi hiki, ukali ambao Mungu alitumia kuzungumza kilikuwa kitu ambacho binadamu hawakuwahi kutarajia na sembuse kusikia, hata hivyo, kujali sana kuhusu hadhi, na juu ya hili, kushughulika kwa msisimko mkubwa na kupata baraka, hawakuwa na wakati wa kuunda fikira kuhusu sauti ya kuzungumza ya Mungu na njia Yake ya kuzungumza, lakini badala yake hali yao wenyewe na kile ambacho siku za usoni zinaweza kuwa nayo, kilajaa akilini mwao. Kwa njia hii, bila kujua, binadamu waliingizwa katika “matata” kwa matamshi ya Mungu aliyokuwa Amewawekea. Wakiwa wameshawishiwa, bila hiari, na mvuto wa siku za mbele na kudura yao, binadamu walijijua kuwa hawafai kuwa nafsi ya Mungu, na bado walikuwa wakisita kutenda kama watendaji huduma Wake. Wakiwa wameshindwa kuchagua kati ya fikira hizi zinazopingana, bila kujijua walikubali hukumu na kuadibu kwa pekee ambako Mungu alikuwa Amewapa binadamu. Kwa kawaida, aina hii ya hukumu na usafishaji kilikuwa kitu ambacho binadamu hawakuwa tayari kukubali hata kidogo. Hata hivyo, Mungu tu ndiye Aliye na hekima, na ni Yeye tu Aliye na uwezo, kuhitaji utii mpole kutoka kwa jamii hii potovu ya wanadamu, ili kwamba, watake au wasitake, wote walikubali mwishowe. Binadamu hawakuwa na njia badala ambazo wangeweza kuchagua. Ni Mungu tu ndiye Aliye na uamuzi wa mwisho, na ni Mungu tu ndiye Anayeweza kutumia mbinu kama hii kumpa mwanadamu ukweli na uhai na kumwonyesha mwelekeo. Mbinu hii ni kutoepukika kwa kazi ya Mungu kwa mwanadamu, na pia, bila shaka au ugomvi, ni

jambo la lazima kwa mwanadamu. Mungu hutumia mbinu kama hii kwa ajili ya kunena na kufanya kazi ili kuwasilisha ukweli huu kwa binadamu: Katika kuwaokoa binadamu, Mungu hufanya hivyo kutokana na upendo na huruma Yake na kwa ajili ya usimamizi Wake; katika kupokea wokovu wa Mungu, jamii ya binadamu hufanya hivyo kwa sababu imeanguka hadi kiwango ambapo Mungu huzungumza binafsi tu. Mwanadamu anapoupokea wokovu wa Mungu, hii ndiyo neema kuu zaidi, na pia ni fadhila ya pekee, yaani, isingekuwa Mungu kulipa sauti tamko Lake mwenyewe, majaliwa ya jamii ya binadamu yangekuwa ni kufa. Wakati huo huo ambapo Anaikirihi jamii ya binadamu, bado Mungu yuko tayari na mwenye radhi kulipa gharama yoyote kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Wakati ule ule, mwanadamu anapozungumza kwa kurudiarudia kuhusu upendo wake kwa Mungu na jinsi anavyoweka yote wakfu kwa Mungu, anaasi dhidi ya Mungu na kupokonya kila aina ya neema kutoka kwa Mungu, huku akimwumiza Mungu na kuutia moyo Wake uchungu mbaya sana. Hivyo ndivyo ilivyo tofauti dhahiri baina ya asiye na ubinafsi na aliye na ubinafsi kati ya Mungu na mwanadamu!

Katika kufanya kazi na kuzungumza, Mungu halazimiki kufuata mbinu yoyote maalum, ila Yeye husababisha kufikia matokeo katika upande Wake. Kwa sababu hii, katika sehemu hii ya matamko Yake, Mungu amehakikisha kutoonyesha utambulisho Wake mwenyewe kwa dhahiri, ila tu kufichua maneno machache kama vile “Kristo wa siku za mwisho,” “Mkuu wa ulimwengu,” na kadhalika. Hili haliathiri huduma ya Kristo au ufahamu wa binadamu kumhusu Mungu hata kidogo, hasa kwa kuwa katika siku hizo za awali binadamu hawakujua kabisa kuhusu dhana ya “Kristo” na “kupata mwili,” kiasi kwamba Mungu alilazimika kujinyenyekeza ili awe mtu aliye na “kazi maalum” ili kuonyesha tamko Lake. Huu ni mfano wa nia yenye juhudi ya Mungu, kwa sababu watu walioishi wakati huo wangeweza tu kukubali aina hii ya mtindo wa mawasiliano. Bila kujali aina ya mtindo wa mawasiliano ambao Mungu hutumia, matokeo ya kazi Yake hayaathiriwi, kwa sababu katika yote anayoyafanya, Mungu hunuia kumwezesha mwanadamu kubadilika, kumwezesha mwanadamu kupata wokovu wa Mungu. Bila kujali Anachokifanya, daima Mungu huyafikiria mahitaji ya mwanadamu. Hii ndiyo nia ya Mungu katika kufanya kazi na kuzungumza. Hata ingawa Mungu yuko mwangalifu kabisa katika kufikiria vipengele vyote vya binadamu, na ni mwenye busara kamili katika yote Anayoyafanya, Ningeweza kusema hili: Kama Mungu hangejishuhudia binafsi, hakungekuwa na yeyote miongoni mwa jamii ya binadamu walioumbwa ambaye anaweza kumtambua Mungu Mwenyewe au kusimama kumshuhudia Mungu Mwenyewe. Kama Mungu angeendelea kutumia “mtu aliye na kazi maalum” kama mtindo wa mawasiliano katika kazi Yake, hakungekuwa na binadamu hata mmoja ambaye angemchukulia Mungu kama Mungu—hii ni huzuni ya binadamu. Yaani, miongoni mwa jamii ya binadamu walioumbwa hakuna ambaye anaweza kumjua Mungu,

sembuse kuwepo na yeyote wa kumpenda Mungu, kumjali Mungu na kumkaribia Mungu. Imani ya mwanadamu ni kwa ajili ya kupata baraka pekee. Utambulisho wa Mungu kama mtu aliye na kazi maalum imetoa dokezo kwa kila binadamu: Binadamu wanaona ikiwa rahisi kumchukulia Mungu kama mmoja miongoni mwa jamii ya wanadamu walioumbwa; uchungu na fedheha kuu kabisa ambayo binadamu wanamwumiza Mungu nayo ni hiyo hasa, Anapoonekana na kufanya kazi waziwazi, bado Mungu anakataliwa na mwanadamu na hata kusahaulika naye. Mungu huvumilia fedheha kuu zaidi ili Aweze kuiokoa jamii ya binadamu; katika kutoa kila kitu, lengo Lake ni kuwaokoa binadamu, ili Aweze kutambuliwa na binadamu. Gharama ambayo Mungu amelipa kwa ajili ya haya yote ni kitu ambacho kila mtu aliye na dhamiri anapaswa kuweza kuthamini sana. Jamii ya binadamu imepata kuzungumza na kufanya kazi kwa Mungu, na kupata wokovu wa Mungu. Hata hivyo, hakuna mtu ambaye amefikiria kuuliza jambo hili: Na ni nini ambacho Mungu amepata kutoka kwa binadamu? Kutoka katika kila tamko la Mungu, binadamu wameupata ukweli, wamefanikiwa kubadilika, wamepata mwelekeo katika maisha; lakini kile ambacho Mungu amekipata si zaidi ya maneno binadamu anayotumia kuonyesha kumdai kwake Mungu na minong’ono dhaifu ya sifa. Hakika hii si fidia ambayo Mungu anadai kutoka kwa mwanadamu?

Ingawa matamko mengi ya Mungu sasa yameonyeshwa, watu wengi sana bado wamesita katika hatua inayowakilishwa na maneno ya Mungu mwanzoni katika ufahamu na maarifa yao kumhusu Mungu, ambapo kwayo hawajaendelea mbele—hili kweli ni swala la kuhuzunisha. Sehemu hii ya “Matamko ya Kristo Mwanzoni” ni ufunguo tu wa kuufungua moyo wa binadamu; kusita hapa ni kutotimiza nia ya Mungu kabisa. Lengo la Mungu katika kunena sehemu hii ya matamko Yake ni kumleta binadamu kutoka kwa Enzi ya Neema hadi katika Enzi ya Ufalme tu; Hataki kamwe binadamu wabaki wakiwa wamesimama katika sehemu hii ya matamko Yake au hata kuchukua sehemu hii ya matamko Yake kama mwongozo, vinginevyo matamko ya baadaye ya Mungu hayatakuwa muhimu au ya maana. Iwapo kuna yeyote ambaye bado hawezi kuingia katika kile ambacho Mungu anadai kwamba mwanadamu anapaswa apate katika sehemu hii ya matamko Yake, basi kuingia kwa mtu huyo kunabaki kitu kisichojulikana. Sehemu hii ya matamko ya Mungu inajumuisha mahitaji ya msingi zaidi ambayo Mungu hutaka kutoka kwa mwanadamu katika Enzi ya Ufalme, na ndiyo njia ya pekee ambayo kwayo binadamu wataingia katika njia sahihi. Iwapo wewe ni mtu asiyelewa chochote, basi ni bora uanze kwa kusoma maneno katika sehemu hii!

Tanbihi:

a. Maandishi ya asili hayana maneno “vikundi tofauti vya.”

Sura ya 1

Sifa zimekuja Sayuni na makazi ya Mungu yameonekana. Jina tukufu takatifu linasifiwa na watu wote, na linaenea. Ah, Mwenyezi Mungu! Mkuu wa ulimwengu, Kristo wa siku za mwisho—Yeye ni Jua linalong’aa, na Ameinuka juu ya Mlima Sayuni ulio na uadhimu na mzuri kabisa katika ulimwengu mzima ...

Mwenyezi Mungu! Sisi tunakushangilia; tunacheza ngoma na kuimba. Kweli Wewe ni Mkombozi wetu, Mfalme mkubwa wa ulimwengu! Umetengeneza kundi la washindi, na kutimiza mpango wa usimamizi wa Mungu. Watu wote wataelekea kwa mlima huu. Watu wote watapiga magoti mbele ya kiti cha enzi! Wewe ndiye Mungu mmoja wa kweli na wa pekee na Unastahili utukufu na heshima. Utukufu wote, sifa, na mamlaka yawe kwa kiti cha enzi! Chemchemi ya maisha hutiririka kutoka kwenye kiti cha enzi, ikinyunyizia na kuwalisha watu wa Mungu. Maisha hubadilika kila siku; nuru mpya na ufunuo hutufuata sisi, daima vikitupatia utambuzi mpya wa Mungu. Kuwa yakini kwa Mungu kupitia uzoefu; maneno Yake daima huonekana, yakionekana kwa wale ambao ni waadilifu. Kwa kweli sisi tumebarikiwa kupita kiasi! Kuwa ana kwa ana na Mungu kila siku, kuwasiliana na Mungu katika kila kitu, na kumpa Mungu mamlaka katika kila kitu. Kwa umakini sisi tunatafakari neno la Mungu, mioyo yetu ni mitulivu katika Mungu, na hivyo sisi tunakuja mbele za Mungu ambapo tunapokea nuru Yake. Katika maisha yetu ya kila siku, matendo, maneno, mawazo, na fikira, tunaishi ndani ya neno la Mungu, na daima tunao utambuzi. Neno la Mungu linapenya; mambo yaliyofichwa ndani kwa ghafula huonekana moja baada ya nyingine. Ushirika na Mungu hauwezi kucheleweshwa; mawazo na fikira huonyeshwa kwa uwazi na Mungu. Kwa kila muda tunaishi mbele ya kiti cha Kristo ambapo sisi hupitia hukumu. Kila eneo la miili yetu linamilikiwa na Shetani. Leo, hekalu la Mungu lazima litakaswe ili Apate ukuu Wake tena. Ili kumilikiwa kabisa na Mungu, ni lazima tupitie vita vya kufa kupona. Ni wakati tu nafsi zetu za zamani zimesulubiwa ndipo maisha ya kufufuliwa ya Kristo yatatawala kwa ukuu.

Sasa Roho Mtakatifu Anafanya shambulio katika kila pembe yetu ili kuzindua vita vya kurudisha! Mradi tuko tayari kujinyima wenyewe na radhi kushirikiana na Mungu, Mungu kwa wakati wowote Ataangaza na kututakasa ndani zetu, na kurudisha upya yale ambayo Shetani amemiliki, ili tuweze kukamilishwa na Mungu haraka iwezekanavyo. Usipoteze muda, na daima uishi ndani ya neno la Mungu. Jengwa pamoja na watakatifu, letwa katika ufalme, na uingie katika utukufu na Mungu.

Sura ya 2

Kanisa la Filadelfia limechukua umbo, na hili limesababishwa kabisa na neema na rehema

za Mungu. Watakatifu wameleta upendo wao wa Mungu mbele na kamwe hawakuyumbayumba kutoka kwa njia yao ya kiroho. Kuwa imara katika imani kwamba Mungu mmoja wa kweli Amekuwa mwili, ya kwamba Yeye ndiye Mkuu wa ulimwengu Ambaye hutawala vitu vyote— hii imethibitishwa na Roho Mtakatifu na ni ushahidi thabiti! Kamwe hauwezi kubadilika!

Eh, Mwenyezi Mungu! Leo Umefungua macho yetu ya kiroho, kuwaruhusu vipofu kuona, viwete kutembea, wenye ukoma kuponywa. Umefungua dirisha la mbinguni na tumeona siri za dunia ya kiroho. Maneno Yako matakatiifu yametujaza sisi, na Umetuokoa kutoka kwa ubinadamu potovu uletwao na Shetani. Hii ni kazi Yako kuu na rehema Yako kubwa sana. Sisi ni mashahidi Wako!

Umekuwa mnyenyekevu na kufichika katika kimya kwa muda mrefu. Wewe umepitia ufufuo na mateso ya msalaba; Wewe umejua furaha na huzuni ya maisha ya binadamu pamoja na mateso na dhiki. Wewe umepitia na kuonja maumivu ya dunia ya binadamu, na Wewe umetelekezwa na enzi. Mungu mwenye mwili ni Mungu Mwenyewe. Wewe umetuokoa kutoka kwa lundo la samadi kwa ajili ya mapenzi ya Mungu na umetushikilia kwa mkono Wako wa kulia; neema Yako imepeanwa huru kwetu sisi. Unafanya juhudi za ukarimu kuingiza maisha Yako ndani yetu; gharama Ulilolipa kwa damu Yako, jasho, na machozi imekuwa katika watakatifu. Sisi ndio matokeo ya^[a] juhudi Zako zenye bidii, sisi ndio gharama Unayolipa.

Eh, Mwenyezi Mungu! Ni kwa sababu ya upendo Wako na rehema, haki Yako na uadhama, utakatifu Wako na unyenyekevu kwamba watu wote wanapaswa kutii mbele Yako na kukuabudu Wewe daima dawamu.

Leo Umefanya kamili makanisa yote—kanisa la Filadelfia—ambayo ni matunda ya miaka 6,000 ya mpango Wako wa usimamizi. Sasa watakatifu kwa unyenyekevu wanaweza kuwa watiifu mbele Yako; wao wameunganishwa pamoja katika roho na kuandama pamoja katika upendo. Wao wameunganishwa kwa chanzo cha chemchemi ya maji. Maji ya uhai ya maisha huenda bila mwisho na husafisha na kutakasa uchafu wote na taka katika kanisa, kwa mara nyingine tena yakitakasa hekalu Lako. Tumemjua Mungu wa ukweli wa vitendo, tumetembea ndani ya maneno Yake, tumetambua shughuli zetu na wajibu wetu wenyewe, na kufanya kila kitu tunachoweza kutumia kila rasilimali yetu kwa ajili ya kanisa. Tunapaswa kuchukua kila muda kuwa kimya mbele Yako na kutilia maanani kazi ya Roho Mtakatifu ili mapenzi Yako yasizuiwe ndani yetu. Miongoni mwa watakatifu kuna upendano, na nguvu za wengine zitafidia dosari za wengine. Tembea katika roho kila muda na upate nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu; fahamu ukweli na uuweke katika vitendo mara moja; kuwa sawa na nuru mpya na kufuata nyayo za Mungu.

Shirikiana kwa utendaji na Mungu; kumruhusu Yeye Achukue uongozi ni kutembea pamoja naye. Mawazo yetu yote wenyewe, fikira na maoni, mitego yetu yote ya kimwili, hutokomea kama moshi. Tunamruhusu Mungu Atawale katika roho zetu, kutembea naye na kupata uwezo unaozidi sana wa mwanadamu, kushinda ulimwengu, na roho zetu huruka kwa uhuru na kufikia ufunguliwaji; haya ni matokeo ya Mwenyezi Mungu kuwa Mfalme. Tunawezaje kukosa kucheza ngoma na kuimba sifa, kutoa sifa zetu, na kutoa nyimbo mpya?

Kweli kuna njia nyingi za kumsifu Mungu: kuliita jina Lake, kukaribia karibu na Yeye, kumfikiria Yeye, kuomba kwa kusoma, na kuwa na ushirika, kuzingatia, kutafakari, na sala, na pia kuna nyimbo za sifa. Katika aina hizi za sifa kuna raha, na kuna kupakwa mafuta; kuna nguvu katika sifa na pia kuna mzigo. Kuna imani katika sifa, na kuna utambuzi mpya.

Shirikiana na Mungu kwa utendaji, tumikia kwa uratibu na kuwa moja, yakidhi mapenzi ya Mwenyezi Mungu, harakisha kuwa mwili mtakatifu wa kiroho, kanyaga Shetani, na kumaliza hatima yake. Kanisa la Filadelfia limechukuliwa kwenda mbinguni mbele ya Mungu na linajidhihirisha katika utukufu wa Mungu.

Tanbihi:

a. Maandishi ya awali hayana maneno “matokeo ya.”

Sura ya 3

Mfalme wa ushindi hukaa juu ya kiti Chake cha enzi cha utukufu. Yeye Ametimiza ukombozi na kuongoza watu Wake wote kuonekana katika utukufu. Yeye hushikilia ulimwengu mikononi Mwake kwa hekima Yake ya uungu na uweza Yeye Amejenga Sayuni na kuifanya imara. Pamoja na uadhama Wake Yeye huhukumu dunia ya maovu; Yeye huhukumu mataifa yote na watu wote, ardhi na bahari na vitu vyote hai ndani yao, pia wale ambao wamelewa kwa divai ya uzinzi. Kwa hakika Mungu atawahukumu hao, na kwa hakika Atakuwa mwenye hasira nao na mle uadhama wa Mungu utafichuliwa. Hukumu ya aina hiyo itakuwa papo hapo na kuwasilishwa bila kuchelewa. Moto ya ghadhabu ya Mungu itachoma makosa yao ya kuchukiza na janga litawafikia wakati wowote; wao hawatajua njia ya kutoroka na hawatakuwa na mahali pa kujificha, wao watalia na kusaga meno yao, na watajiletea maangamizi.

Wana wa ushindi wapendwa wa Mungu kwa hakika watakaa katika Uyahudi, kamwe wasiiache. Umati utasikiliza sauti Yake kwa makini, watatilia maanani kwa uangalifu matendo Yake, na sauti zao za sifa Kwake kamwe hazitakoma. Mungu mmoja wa kweli Ameonekana! Tutakuwa na uhakika juu Yake katika roho na kumfuata kwa karibu na kukazana kusonga mbele bila kusita. Mwisho wa dunia unajitokeza mbele yetu; maisha sahihi ya kanisa pamoja na watu, shughuli, na mambo ambayo yanatuzunguka sasa hata yanayafanya mafunzo yetu yawe makali

zaidi. Acha tufanye hima kuchukua tena mioyo yetu ambayo inapenda dunia sana! Acha tufanye hima kuchukua tena maono yetu yaliyozibwa! Hatutasonga mbele zaidi tusije tukazidi mipaka na tutashikilia ndimi zetu ili tuweze kuishi kwa kufuata neno la Mungu, na tena hatutazozana juu ya faida zetu wenyewe na hasara. Acha upendo wako wa dunia ya kawaida na utajiri! Ah, jiwekeni huru kutoka kwake—upendo wenu wa kuning'nia kwa waume zenu na mabinti na wana wenu! Acha maoni yako na upendeleo! Amka, kwa sababu muda ni mfupi! Iruhusu roho yako iangalie juu, angalia juu na umruhusu Mungu Achukue uongozi. Usijiruhusu kuwa kama mke wa Lutu. Kutelekezwa ni jambo la kusikitisha sana! Ni la kusikitisha kweli! Amka!

Sura ya 4

Muda baada ya mwingine, tutakuwa tunakesha na kusubiri, kuwa na utulivu katika roho na kutafuta kwa moyo safi. Chochote kitakachotufikia, tusishiriki kwa upofu. Twahitajika tu kuwa kimya mbele ya Mungu na daima kushiriki naye, na kisha nia Yake itafichuliwa kwetu. Roho zetu sharti daima ziwe tayari kutofautisha na sharti ziwe na bidii na zisiokubali kushindwa. Ni lazima tuteke kutoka kwa maji ya uhai mbele ya Mungu, maji yanayozilisha na kuzirutubisha roho zetu zilizo na kiu. Ni lazima tuwe tayari wakati wowote, kujitakasa kutokana na haki ya kibinafsi, kiburi chetu, kujiridhisha kibinafsi, na ridhaa yetu, kila moja kuzaliwa kutoka kwa tabia yetu ya kishetani. Ni sharti tufungue mioyo yetu ili kukubali neno la Mungu, sharti tutumainie maneno Yake tunapojishughulisha na maisha yetu. Ni lazima tupitie na tuwe na uhakika juu ya neno Lake na kutimiza ufahamu wa neno Lake, tukiruhusu neno Lake kuwa maisha yetu. Huu ni wito wetu! Sisi hushinda tu tunapoishi kwa maneno ya Mungu.

Sasa dhana zetu ni kali sana, sisi husema kwa wepesi na kuchukua hatua kwa pupa na hatuwezi kufuata Roho. Leo haitakuwa kama zamani; kazi ya Roho Mtakatifu husonga mbele kwa kasi kubwa. Sharti tupitie neno la Mungu kwa undani; kila wazo na fikira, kila mwendo na jibu ni lazima tutofautishe miyoyoni mwetu. Hakuna tunachofanya mbele ya mtu au nyuma yao yanaweza kutoroka hukumu mbele ya kiti cha Kristo. Roho Mtakatifu anatuongoza katika maeneo ya uzoefu zaidi, na kwa njia hii ya uzoefu tunakaribia kuwa na uhakika juu ya mwenye Uweza.

Mungu wa ulimwengu Amefungua macho yetu ya kiroho na siri katika roho huendelea kufichuliwa kwetu. Tafuta kwa moyo safi! Kuwa tayari kulipa gharama, songa mbele kwa moyo wako wote, kuwa tayari kujinyima, usiwe na tamaa tena, fuata Roho Mtakatifu na furahia neno la Mungu na kwa ujumla mtu mpya ataonekana. Wakati umewadia, ambapo Shetani atafikia kikomo chake, mapenzi ya Mungu yatatendeka. Mataifa yote ya dunia yatakuwa Ufalme wa Kristo na Kristo Atatawala kama Mfalme duniani milele!

Sura ya 5

Milima na mito huenda ikibadilika, vijito hutiririka kwenye mikondo yao, na maisha ya mwanadamu ni yenye uvumilivu mdogo kuliko ardhi na anga. Mwenyezi Mungu pekee ndiye maisha ya milele yaliyofufuka milele, katika vizazi hai milele! Vitu vyote na matukio viko katika mikono Yake, Shetani yuko chini ya miguu Yake.

Leo hii ni kwa sababu ya uteuzi wa Mungu ulioamuliwa kabla kwamba Ametuokoa kutoka kukamatwa na Shetani. Yeye kweli ni Mkombozi wetu. Maisha ya kufufuliwa ya Kristo milele yametugusa ndani yetu, hivi sisi tumejaliwa kuhusiana na maisha ya Mungu, tunaweza kuwa naye ana kwa ana, kumla Yeye, kumnywa Yeye, na kumfurahia Yeye. Huku ni kujitolea kwa Mungu kwa bidi na kusio na ubinafsi.

Majira yanakuja na ku kuenda, yakipitia upepo na jalidi, yakikumbana na taabu, mateso na majonzi mengi sana ya maisha, kukataliwa na kukashifiwa duniani, serikali kusingizia mashtaka, hakuna upungufu wa imani ya Mungu wala kusudi. Kwa ukamilifu kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, ili usimamizi wa Mungu na mpango utimizwe, Yeye huweka maisha Yake Mwenyewe kando. Kwa ajili ya watu Wake wote, huwa Hapuri juhudi yoyote, kwa uangalifu Akilisha na kunyunyizia. Haidhuru kiasi cha ujinga, tu wagumu kiasi kipi, tunahitaji tu kutii mbele Yake, na maisha ya kufufuka kwa Kristo yatabadilisha asili yetu ya zamani.... Kwa wana hawa wazaliwa wa kwanza, Yeye hufanya kazi bila kuchoka, huachilia chakula na usingizi. Ni mchana na usiku ngapi, ni kupitia joto ngapi kali, na baridi ya kuganda, Yeye hutazama kwa moyo mmoja katika Sayuni.

Ulimwengu, nyumba, kazi vimeachiliwa kabisa, bila kusita, bila raha za kidunia kumgusa.... Maneno kutoka kinywa Chake yanatupiga kwa ndani, yakifunua mambo yaliofichwa kwenye kina cha mioyo yetu. Ni vipi haturidhishwi? Kila sentensi inayotoka katika kinywa Chake inatendeka wakati wowote kwetu. Kila kitendo chetu, hadharani na faraghani, hakuna ambacho Yeye hakijui, hakuna Asichokijua. Kwa kweli vyote vitafichuliwa mbele Yake, licha ya mipango yetu wenyewe na matayarisho.

Tukiwa tumeketi mbele Yake, roho zetu hufurahia, kustareheshwa na tulivu, daima kuhisi tupu ndani, kwa kweli kuwiwa kwa Mungu. Hili ni jambo la ajabu lisilofikirika na lisiloweza kufanikishwa. Roho Mtakatifu anathibitisha vya kutosha kwamba Mwenyezi Mungu ni Mungu mmoja wa kweli! Asiyepingika! Sisi, kundi hili la watu, kwa kweli tumebarikiwa! Kama si kwa neema ya Mungu na rehema, lazima tuangamie milele na kumfuata Shetani. Ni Mungu Mwenyezi pekee Anayeweza kutuokoa!

Ah! Mwenyezi Mungu, Mungu wa vitendo! Ni Wewe ambaye Umefungua macho yetu ya

kiroho, kwamba tumeweza kuona siri za dunia ya kiroho. Taswira za ufalme hazina na mwisho. Kuweni waangalifu na wenye kusubiri. Siku haiwezi kuwa mbali sana.

Mioto ya vita huzunguka, moshi wa bunduki huelekea, hali ya hewa huwa vuguvugu, tabia ya nchi hubadilika, tauni litaenea, na watu lazima wafariki, na tumaini ndogo la kuishi.

Ah! Mwenyezi Mungu, Mungu wa vitendo! Wewe ni mnara wetu imara. Wewe ni kimbilio letu. Sisi tunakusanyika chini ya mabawa Yako, na janga haliwezi kutufikia. Huu ni utunzaji Wako mtakatifu.

Sisi sote tunainua sauti zetu, kuimba sifa, sifa ambazo zinavuma kote Sayuni! Mwenyezi Mungu, Mungu wa vitendo ameandaa hatima hio tukufu kwa ajili yetu. Kuwa mwangalifu—mwangalifu! Wakati hauwezi kuwa mbali sana.

Sura ya 6

Mwenyezi Mungu, Mkuu wa vitu vyote, hushika madaraka Yake ya kifalme kutoka kwa kiti Chake cha enzi. Yeye hutawala ulimwengu na vitu vyote na Yeye yuko katika harakati ya kutuongoza katika dunia yote. Kila wakati tutakuwa karibu na Yeye, na kuja mbele Zake kwa utulivu; kamwe hatutakosa wakati mmoja, na kuna mambo ya kujifunza wakati wote. Mazingira yanayotuzunguka pamoja na watu, mambo na vitu, yote yameruhusiwa na kiti Chake cha enzi. Usiwe na moyo wa kunung'unika, au Mungu hatatupa neema Yake juu yako. Wakati ugonjwa hutokea ni kwa sababu ya upendo wa Mungu, na nia Yake nzuri kwa hakika inaiunga mkono. Hata wakati mwili wako unavumilia mateso, usichukue ushauri kutoka kwa Shetani. Sifu Mungu katikati ya ugonjwa na furahia Mungu katikati ya sifa yako. Usikate tamaa unapokabiliwa na ugonjwa, endelea kutafuta na kamwe usisalimu amri, na Mungu Ataangaza nuru Yake kwako. Ayubu alikuwa mwaminifu kiasi gani? Mwenyezi Mungu ni daktari mwenye nguvu zote! Kukaa katika ugonjwa ni kuwa mgonjwa, lakini kukaa katika roho ni kuwa mzima. Kama unayo pumzi moja tu, Mungu hatakuacha ufariiki.

Ndani yetu tuna uzima wa Kristo Aliyefufuka. Bila shaka, hatuna imani mbele ya Mungu: Na iwe kwamba Mungu Atie imani ya kweli ndani yetu. Neno la Mungu ni tamu kweli! Neno la Mungu ni dawa yenye nguvu! Tilia aibu mapepo na Shetani! Kama sisi tutafahamu neno la Mungu tutakuwa na msaada na neno Lake litaokoa mioyo yetu kwa haraka! Linaondoa vitu vyote na kuweka yote kwa amani. Imani ni kama daraja moja la gogo la mti, wale ambao hushikilia maisha kwa unyonge watakuwa na ugumu katika kulivuka, lakini wale ambao wako tayari kujitolea wenyewe wanaweza kulivuka bila wasiwasi. Kama mtu ana mawazo ya uoga na ya kuogofya, wao wanadanganywa na Shetani. Ina hofu kwamba tutavuka daraja la imani ili kuingia katika Mungu. Shetani hubuni kila njia iwezekanayo kututumia mawazo yake,

tunapaswa daima kuomba kwamba nuru ya Mungu itatuangazia sisi, na ni lazima daima tumtumainie Mungu kututakasa kutoka kwa sumu ya shetani. Daima tutakuwa tukitenda katika roho zetu kuja karibu na Mungu. Tutamruhusu Mungu kuwa na utawala juu ya asili yetu yote.

Sura ya 7

Kuinuka kwa mazingira pande zetu zote huharakisha kurudi nyuma kwetu katika roho. Usitende kwa moyo mgumu, usipuuze kwa vyovyote vile kama Roho Mtakatifu Ana wasiwasi, usijaribu kuwa mjanja na usiwe na ridhaa kupita kiasi na kuridhika kibinafsi au kuzingatia sana matatizo yako mwenyewe; kitu pekee cha kufanya ni kumwabudu Mungu katika roho na kweli. Huwezi kuyaacha maneno ya Mungu nyuma au kuyapa kisogo; lazima uyaelewe kwa makini, rudia kuomba-kusoma kwako, na uelewe maisha ndani ya maneno hayo. Usishiriki katika yale yasiyokuwa na maana kwa kuyabugia pasipo kujipa mwenyewe wakati wa kuyawaza. Je, unategemea maneno ya Mungu kwa kila kitu unachofanya? Usizungumze makubwa kama mtoto na kisha ukuwe katika mvurugo wakati wowote kitu chochote kinazuka. Lazima utumie roho yako kila saa ya kila siku, usipumzike hata kwa muda. Lazima uwe na roho yenye makali. Haijalishi ni mtu, tukio au kitu gani unachoweza kukumbana nacho, ukija mbele ya Mungu utakuwa na njia ya kufuata. Lazima ule na kunywa maneno ya Mungu kila siku, uelewe maneno Yake bila kuwa na uzembe, ufanye juhudi zaidi, upate kabisa kila maelezo na kujiandaa mwenyewe na ukweli kamili ili kuepukana na kutoelewa mapenzi ya Mungu. Ni lazima upanue safu zako za uzoefu na ulenge kupitia maneno ya Mungu. Kupitia uzoefu utakuwa na uwezo wa kuwa yakini zaidi kuhusu Mungu; bila uzoefu, kusema u yakini juu Yake ni maneno tu tupu. Ni lazima tuwe wenye kuelewa haraka! Amka! Usiwe mlegevu tena; ukikabiliana na mambo kwa njia paruparu na wala hautajitahidi kwa maendeleo basi kwa kweli wewe ni kipofu. Ni lazima ulenge kazi ya Roho Mtakatifu, sikiza kwa makini sauti ya Roho Mtakatifu, fungua masikio yako kwa maneno ya Mungu, tunza muda uliobaki na ulipe gharama, hata iwe ni gani. Ukiwa na chuma cha pua, kitumie pahali kinapofaa zaidi—kutengeneza upanga thabiti; shikilia kwa uthabiti kile kilicho muhimu na ulenge kuweka maneno ya Mungu katika vitendo. Ukiwa umeyaacha maneno ya Mungu, basi haijalishi unavyoweza kufanya vizuri kwa nje, yote itakuwa ni bure. Kutenda kwa maneno matupu tu haikubaliki kwa Mungu; mabadiliko lazima yaje kwa njia ya mwenendo wako, tabia, imani, ujasiri na utambuzi.

Wakati u karibu sana! Haidhuru mambo ya dunia ni mazuri kiasi kipi, ni lazima yote yaachwe kando. Matatizo mengi na hatari hayawezi kutuogofya sisi, wala anga kuanguka hakutatushinda kabisa. Bila aina hii ya azimio itakuwa ngumu tu sana kwako wewe kuwa mtu yeyote wa umuhimu. Wale ambao ni wadhaifu na ambao kwa uoga hushikilia maisha hawastahili kusimama mbele ya Mungu.

Mwenyezi Mungu ni Mungu wa vitendo. Haidhuru jinsi tu wapumbavu, Yeye bado Atatuonea huruma, mikono Yake hakika itatuokoa sisi na bado Atatufanya kamili. Mradi tuna moyo ambao kwa kweli unamtaka Mungu, mradi tumfuate karibu na wala tusikatishwe tamaa, na tutafute kwa hisia ya haraka, basi kwa hakika Hatachukulia yeyote kati yetu bila haki, kwa hakika Atatufidia sisi kile ambacho tuna ukosefu nacho na Yeye Ataturidhisha—yote hii ni wema wa Mwenyezi Mungu.

Kama mtu ni mlafi na mvivu, anaongoza maisha shibe, legevu na hajali chochote, yeye atapata kuwa ni vigumu kuepuka kupata hasara. Mwenyezi Mungu Hutawala mambo yote na matukio yote! Mradi tunamtegemea mioyoni mwetu kila wakati na tuingie rohoni na kufanya ushirika na Yeye, basi Atatuonyesha mambo yote tunayotafuta na mapenzi Yake kwa hakika yatafichuliwa kwetu; mioyo yetu kisha yatakuwa katika furaha na amani, thabiti kwa uwazi kamili. Ni muhimu kuwa na uwezo wa kutenda kulingana na maneno Yake; kuwa na uwezo wa kuelewa mapenzi Yake na kuishi katika utegemezi wa maneno Yake—hii tu ndiyo kupitia kwa kweli.

Ni kwa kuelewa tu maneno ya Mungu ndipo ukweli wa maneno Yake utaweza kuingia ndani yetu na kuwa maisha yetu. Bila kupitia kwa vitendo vyovyote, unawezaje kuingia kwa uhalisi wa maneno ya Mungu? Kama huwezi kupata maneno ya Mungu kama maisha yako basi tabia yako haitaweza kubadilika.

Kazi ya Roho Mtakatifu sasa inaendelea kwa upesi sana! Kama haufuati kwa karibu na kupokea mafunzo, itakuwa vigumu kuwa sawa na kuendelea kwa kasi kwa Roho Mtakatifu. Harakisha na usababishe mabadiliko ya kimsingi usije ukakanyagwa chini ya miguu na Shetani na kuingia katika ziwa la moto wa jahanamu ambako hakuna kutoroka. Nenda tafuta kadri unavyoweza sasa ili usitelekezwe.

Sura ya 8

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu—Mfalme wa ufalme—ameshuhudiwa, mawanda ya usimamizi wa Mungu yamejitokeza kabisa katika ulimwengu wote. Sio tu kwamba kuonekana kwa Mungu kumeshuhudiwa nchini China, lakini jina la Mwenyezi Mungu limeshuhudiwa katika mataifa yote na nchi zote. Wote wanaliita jina hili takatifu, wakitafuta kufanya ushirika na Mungu kwa njia yoyote iwezekanayo, wakiyafumbata mapenzi ya Mwenyezi Mungu na kuhudumu kwa uratibu katika kanisa. Roho Mtakatifu hufanya kazi kwa njia hii ya ajabu.

Lugha za mataifa mbalimbali ni tofauti na kila nyingine lakini kuna Roho mmoja tu. Huyu Roho huunganisha makanisa kote ulimwenguni na ni mmoja na Mungu, bila tofauti hata kidogo, na hili ni jambo ambalo halina shaka kabisa. Roho Mtakatifu sasa anawapaazia sauti na sauti

Yake yawaamsha. Hii ni sauti ya huruma ya Mungu. Wanaliita kwa sauti jina takatifu la Mwenyezi Mungu! Wao pia wanatoa sifa na kuimba. Hakuwezi kuwa na mkengeuko wowote katika kazi ya Roho Mtakatifu, na watu hawa hufanya linalowezezekana ili kuendelea kwenye njia sahihi, huwa hawajitoi na maajabu yake hulundikana juu ya maajabu. Ni kitu ambacho watu huona ugumu kufikiria na kisichowezezekana kukikisia.

Mwenyezi Mungu ndiye Mfalme wa maisha katika ulimwengu! Yeye huketi juu ya kiti kitukufu cha enzi na huihukumu dunia, huwatawala wote, huyaongoza mataifa yote; watu wote hupiga magoti Kwake, humwomba, huja karibu naye na kuwasiliana na Yeye. Bila kujali muda gani mmemwamini Mungu, jinsi hadhi yenu ilivyo ya juu au jinsi ukubwa wenu wa vyeo ulivyo, kama nyinyi humpinga Mungu katika mioyo yenu basi ni lazima mhukumiwe na lazima msujudu mbele Yake, mkitoa sauti chungu ya kusihi kwenu; huku kweli ni kuvuna matunda ya matendo yenu wenyewe. Sauti hii ya kupiga mayowe ni sauti ya kuteswa katika ziwa la moto na kiberiti, na ni kilio cha kuadibiwa na fimbo ya chuma ya Mungu; hii ndiyo hukumu mbele ya kiti cha Kristo.

Baadhi ya watu huogopa, baadhi huficha dhamiri zenye hatia, baadhi wako macho, baadhi huwa waangalifu kusikiza kwa makini, baadhi hutubu na kuanza upya, wakihisi majuto makubwa sana, baadhi hulia kwa uchungu na maumivu, baadhi huachilia kila kitu na kutafuta bila tumaini, baadhi ya watu hujichunguza wenyewe na hawathubutu kutenda bila mpango tena, baadhi hujaribu kwa haraka kuwa karibu na Mungu, baadhi huchunguza dhamiri zao wenyewe, wakijiuliza kwa nini maisha yao hayawezi kuendelea. Baadhi hubaki katika mkanganyiko, baadhi hujifungua pingu za miguu yao na kusonga mbele kwa ushujaa, wakishika ufunguo na kutopoteza wakati kuzingatia maisha yao. Baadhi bado husita na hawako wazi juu ya maono—mzigo walio nao na wanaoubeba katika mioyo yao ni mzito kweli kweli.

Kama mawazo yako si wazi basi Roho Mtakatifu hana njia ya kufanya kazi ndani yako. Yote unayoyazingatia, njia unayoitembea na yote ambayo moyo wako unatamania sana yamejawa na dhana zako na wazo lako la uadilifu wa kibinafsi! Mimi nawashwa na ukosefu wa subira—jinsi Mimi natamani kuwa Ningewafanya nyote wakamilifu moja kwa moja hivi karibuni ili muwe wa faida Kwangu na mzigo Wangu mzito unaweza kufanywa mwepesi. Lakini kwa kuwaangalia nyinyi, Mimi naona ni muhali kuwa na shauku juu ya matokeo. Naweza tu kusubiri kwa ustahimilivu, nitembee polepole na kuwasaidia polepole na kuwaongoza. Ah, lazima mviweke vichwa vyenu wazi! Ni kipi kinachopaswa kutelekezwa, hazina zako ni zipi, udhaifu wako ni upi, vikwazo vyako ni vipi, zielewe zaidi katika roho yako na ufanye ushirika na Mimi zaidi. Kile Ninachotaka ni kwa nyoyo zenu zinitegemee Mimi kwa unyamavu, si kuniunga mkono kinafiki. Wale ambao kwa kweli hutafuta mbele Yangu, Nitayafichua yote kwako. Kasi

Yangu huongezeka mwendo; bora moyo wako hunitegemea Mimi na wewe hufuata wakati wote basi mapenzi Yangu unaweza kupewa wewe kwa msukumo na kufichuliwa kwako wakati wowote. Wale wanaotahadhari kusubiri watapata chakula na watakuwa na njia ya kwenda mbele. Wale wasiojali wataona ugumu wa kuuelewa moyo Wangu, na watafikia mwisho kabisa.

Mimi natamani nyinyi muinuke haraka na kushirikiana na Mimi, na muwe karibu na Mimi wakati wote, siyo tu kwa siku moja na usiku mmoja. Mkono Wangu ni lazima daima uwavute na kuwachochea, kuwaendeleza kwa nguvu, kuwashawishi kuendelea na kuwasihi ili mwendelee! Nyinyi hamuelewi kabisa mapenzi Yangu. Vizuizi vya fikira zenu wenyewe na vizuizi vya matatizo ya dunia ni makali mno, na hamna uwezo kuwa karibu zaidi na Mimi. Kusema kweli, nyinyi huja Kwangu wakati mna hoja, lakini wakati hamna hoja yoyote mawazo yenu huwa na mahangaiko. Yanakuwa kama soko huru na yamejawa na tabia ya kishetani, nyoyo zenu zinamilikiwa na mambo ya kidunia na hamjui jinsi ya kufanya ushirika na Mimi. Ningekosaje Mimi kuwahangaikia? Lakini haitasaidia kuhangaika. Muda umeyoyoma sana na kazi hii inahitaji nguvu nyingi. Hatua Zangu zaruka kuelekea mbele; lazima mshikilie imara yote mliyo nayo, nitumainieni Mimi kila wakati, fanyeni ushirika wa ndani na Mimi na mapenzi Yangu kwa hakika yatafichuliwa kwako wakati wowote. Mnapouelewa moyo Wangu basi mna njia ya kwenda mbele. Lazima msisite tena. Shikilia ushirika wa kweli na Mimi, na usiishie kudanganya au kujaribu kuwa mwerevu sana; huko kutakuwa ni kujidanganya wenyewe tu na kutafichuliwa wakati wowote mbele ya kiti cha Kristo. Dhahabu halisi haiogopi kujaribiwa na moto—huu ndio ukweli! Usione haya, usivunjike moyo au kuwa dhaifu. Fanya ushirika na Mimi moja kwa moja katika roho yako, subiri kwa ustahimilivu na Mimi kwa hakika Nitakufichulia kulingana na wakati Wangu. Wewe kweli, lazima kabisa utahadhari na usiache juhudi Zangu zipotelee bure kwako, na usipoteze wakati. Wakati moyo wako una ushirika na Mimi daima, wakati moyo wako huishi daima mbele Yangu, basi hakuna mtu, hakuna tukio hakuna kitu, hakuna mume, hakuna mwana au binti anayeweza kuvuruga ushirika wako na Mimi ndani ya moyo wako. Wakati moyo wako unawekewa mipaka daima na Roho Mtakatifu na wakati unafanya ushirika na Mimi kila wakati, mapenzi Yangu kwa hakika yatafichuliwa kwako. Wakati unapojongea karibu na Mimi daima kwa njia hii, bila kujali mazingira yako au upo kwa wakati upi maalum, basi huwezi kuvurugika bila kujali ni nani au ni nini unachokabili, na wewe utakuwa na njia ya kwenda mbele.

Kama kwa kawaida huachi chochote kiteleze katika mambo makubwa au madogo, kama moyo wako na mawazo yako yametakaswa, na kama wewe ni mtulivu katika roho yako, basi wakati unapokutana na suala fulani maneno Yangu mara moja yatakuwa na msukumo ndani yako, kama kioo chenye kung'aa kwako kujiangalia mwenyewe kwacho, na wewe ndipo utakapokuwa na njia ya kwenda mbele. Hii inaitwa kuwa na dawa sahihi kwa hali sahihi! Na hali

yoyote kwa hakika itatibiwa—Mungu ni mwenyezi hivi. Kwa hakika Mimi nitawaangazia na kuwapa nuru wale wote wenye njaa na kiu ya haki na ambao hutafuta kwa uaminifu. Mimi nitawaonyesha ninyi nyote siri za ulimwengu wa kiroho na kuonyesha njia ya kwenda mbele, Niwafanye mtupilie mbali tabia zenu mbovu za zamani haraka iwezekanavyo na mfikie ukomavu wa maisha ili kwamba muweze kuwa na manufaa Kwangu, na kwamba kazi ya injili hivi karibuni itaendelea bila kizuizi. Ni hapo tu mapenzi Yangu yatakaporidhishwa, ni hapo tu ndipo mpango wa usimamizi wa Mungu wa miaka elfu sita utatimizwa haraka iwezekanavyo. Mungu ataupata ufalme na atakuja chini duniani, na kwa pamoja tutaingia katika utukufu!

Sura ya 9

Nataka kukukumbusha kwamba huwezi kuwa na wasiwasi hata kidogo juu ya neno Langu na kutokujali kwa aina yoyote hakukubaliki. Unapaswa kulisikiliza na kulitii na kutenda mambo kulingana na nia Zangu. Daima lazima uwe macho na kamwe usiwe na tabia ambayo ni ya kiburi na ya kujidai, na lazima kila wakati unitegemee Mimi ili kutupilia mbali tabia ya zamani ya asili ambayo hukaa ndani yako. Unapaswa daima kuwa na uwezo wa kudumisha hali ya kawaida mbele Yangu, na uwe na tabia thabiti. Kuwaza kwako lazima kuwe kwa busara na wazi na hakupaswi kuyumbishwa au kudhibitiwa na mtu yeyote, tukio, au kitu. Unapaswa kuwa mtulivu daima katika uwepo wangu na daima udumishe ukaribu wa kuendelea na kushiriki na Mimi. Ni sharti uonyeshe nguvu na ukakamavu na usimame imara katika ushahidi wako Kwangu. Simama na kuzungumza kwa ajili Yangu na usiogope kile ambacho watu wengine wanasema. Zingatia kukidhi nia Zangu na usidhibitiwe na wengine. Kile Ninachokufichulia lazima kifanywe kwa mujibu wa nia Zangu na hakiwezi kucheleweshwa. Je, unajihisi vipi ndani yako? Je! una wasiwasi? Utaelewa. Kwa nini huwezi kusimama kuzungumza kwa ajili yangu na kufikiria juu ya mzigo Wangu? Unaendelea kujihusisha na hila ndogo, lakini ninayaona yote kwa uwazi. Mimi ni msaada wako na kinga yako, na vyote viko mikononi Mwangu, hivyo unaogopa nini? Je, huko sio kuwa na mhemuko sana? Lazima utupilie kando hisia haraka sana; Sitendi kwa kufuata muhemko, bali Ninatenda haki badala yake. Wazazi wako wakifanya chochote kisicho na faida kwa kanisa, hawawezi kuepuka. Nia Zangu zimefichuliwa kwako na hupaswi kuzipuuzia. Badala yake, lazima uweke uangalifu wako wote katika hayo na kutupa kila kitu kando ili kufuata kwa moyo wako wote. Mimi nitakuweka mikononi Mwangu siku zote. Usiwe mwoga na kudhibitiwa na mume au mke wako; utaruhusu mapenzi Yangu kufanywa.

Kuwa na imani! Kuwa na imani! Mimi ni mwenyezi wako. Hiki ni kitu ambacho unaweza ukakitambua kiasi, lakini bado unapaswa kutahadhari. Kwa ajili ya kanisa, mapenzi Yangu, na usimamizi Wangu, lazima ujitoe kikamilifu, na siri zote na miisho yote itaonyeshwa kwako. Hakutakuwa na uchelewaji zaidi na siku zitafikia mwisho. Kwa hiyo utafanya nini? Unawezaje

kutafuta kuyafanya maisha yako yakomae kwa kasi zaidi? Je! Utafanyika mwenye manufaa Kwangu haraka kiasi gani? Utafanyaje ili mapenzi Yangu yatekelezwe? Ili kufanya hivyo kunahitaji kutafakari kikamili na ushirika wa kina zaidi na Mimi. Nitegemee Mimi, niamini Mimi, usiwe mzembe kamwe, na uweze kufanya mambo kulingana na mwongozo Wangu. Ukweli lazima utayarishwe vizuri na unapaswa kuula na kuunywa mara kwa mara zaidi. Kila ukweli lazima utekelezwe kabla ya kueleweka vizuri.

Je, sasa unahisi hakuna muda wa kutosha? Je, wewe pia unahisi kuwa u tofauti ndani ukilinganishwa na kabla na kwamba mzigo wako unaonekana kuwa mzito sana? Nia zangu ni juu yako; lazima uelewe waziwazi, usiende mbali nazo, na daima uunganike na Mimi. Kaeni karibu na Mimi daima, wasilianeni na Mimi, muwe wenye kufikiria moyo Wangu, na kuwa na uwezo wa kuhudumu katika ushirikiano, ili nia Zangu zifichuliwe kwenu. Daima zingatia kwa karibu! Uangalifu wa karibu! Usizembe hata kidogo; huo ni wajibu wako na kazi Yangu hukaa ndani yake.

Unaweza kuwa na ufahamu mdogo katika hatua hii na ukajihisi kuwa hii ni ajabu sana. Huenda ulikuwa na mashaka katika siku za nyuma na ukahisi kuwa ilikuwa tofauti kabisa na dhana, mawazo, na fikra za mwanadamu, lakini wewe unaelewa kimsingi kwa sasa. Hii ni kazi Yangu ya ajabu na ni kazi ya ajabu ya Mungu pia. Lazima uwe macho kabisa na usubiri na kutembea ndani yake. Muda uko mikononi Mwangu; usiupoteze, na kamwe usizembe hata kwa muda mchache; kupoteza muda kunachelewesha kazi Yangu na kunasababisha mapenzi Yangu yazuiwe ndani yako. Lazima ufikirie na uwasiliane na Mimi mara kwa mara. Lazima ulete matendo yote, harakati, fikra, mawazo, familia, mume, wana na mabinti mbele Yangu. Usijitegemee mwenyewe katika matendo yako, vinginevyo Nitakuwa na hasira na hasara zako zitakuwa ghali.

Zizuie hatua zako mwenyewe wakati wote na uwe na uwezo wa kutembea ndani ya maneno Yangu daima. Itawezekana tu ikiwa una hekima Yangu. Njoo mbele Yangu ikiwa unakabiliwa na shida na nitakupa mwongozo. Usifanye fujo na kuwasiliana bila kujali. Ikiwa maisha yako hayapati faida ni kwa sababu hauna ujuzi na hauwezi kutofautisha kati ya maneno mazuri na mabaya. Hutambui hili mpaka udhuriwe na hali zenu ni duni, na huna uwepo wa Roho Mtakatifu. Kwa wakati huo, unakuwa umechelewa sana. Muda unasonga sana sasa, hivyo hupaswi kusalia nyuma hata kidogo katika mbio za maisha yako; lazima ufuate hatua Zangu kwa karibu. Wakati shida zozote zinapotokea, fikiria mara kwa mara kupitia kukaa karibu na Mimi na kuwasiliana Nami moja kwa moja. Ikiwa unaelewa njia hii, kuingia kwako kutakuwa rahisi wakati unavyoendelea kusonga mbele.

Maneno Yangu hayaelekezwi kwako tu; kila mtu kanisani amepungukiwa katika vipengele

tofauti tofauti. Lazima muwasiliane zaidi, muweze kula na kunywa kwa kujitegemea wakati wa ibada zenu za kiroho, na muweze kuelewa ukweli muhimu wa kutia katika vitendo mara moja. Lazima uweze kuhisi uhalisi wa neno Langu. Elewa kiini chake na kanuni zake kabisa; usizembe. Litafakari neno Langu daima na uwasiliane nami daima, na hatua kwa hatua litafichuliwa. Huwezi kuja karibu na Mungu kwa wakati kidogo na kisha kabla moyo wako unaweza kuwa na utulivu mbele ya Mungu, usumbuliwe pale vitu vingine vitakapokutokea. Wewe daima unachanganyikiwa na hauna uhakika juu ya mambo na hauwezi kuuona uso Wangu, hivyo hauwezi kuelewa vizuri Moyo wangu. Hata kama unaweza kuelewa kidogo huna uhakika na bado una shaka. Mpaka pale nitakapomiliki moyo wako kwa ukamilifu na akili zako hazisumbuliwi tena na mambo yote ya kidunia, na unaposubiria kwa akili zilizo wazi na zenye utulivu—ndipo wakati ambao, nitawafichulia, kidogo kidogo, kwa mujibu wa nia Zangu. Mnapaswa kuelewa njia hii ya kuwa karibu na Mimi. Yeyote anayekupiga au kukulaani, au jinsi gani vitu wanavyokupa watu vilivyo vizuri, havikubaliki ikiwa vinakufanya kutokuwa karibu na Mungu. Acha moyo wako uwe ndani ya mshiko Wangu na usiniache kamwe. Kwa aina hii ya ukaribu na ushirika, bila kujali kama ni wazazi wako, mume, watoto, mahusiano mengine ya kifamilia, au vifungo vya kidunia, vyote vitaondoka. Utafurahia utamu ambao ni karibu na usioelezeka ndani ya moyo wako na utapitia ladha ya harufu nzuri na utamu mzuri, na hakika hutatengeka kutoka Kwangu. Ikiwa daima ni kama hivi, mtalewa yaliyo ndani ya moyo Wangu. Kamwe hamtapoteza njia yenu mtakavyokuwa mnaendelea mbele, kwa maana Mimi ni njia yenu, na kila kitu kipo kwa sababu Yangu. Jinsi maisha yako yamekomaa, lini utaweza kuwa huru dhidi ya ulimwengu huu, lini utaweza kutupilia mbali hisia zako, lini utaweza kuwaacha nyuma mume wako na watoto, maisha yako yatakoma lini ... mambo haya yote yatafanyika kulingana na wakati Wangu. Hakuna haja ya kuwa na wasiwasi.

Lazima uingie kutokea upande mzuri. Ikiwa unasubiri kwa kukaa tu, bado ni hasi. Lazima uwe wa vitendo katika kushirikiana na Mimi; kuwa na bidii na usiwe mvivu kamwe. Daima uwe katika ushirika na Mimi na uwe na urafiki wa kina sana na Mimi. Ikiwa huelewi, usikose subira kwa ajili ya matokeo ya haraka. Sio kwamba sitakuambia, Ninataka kuona ikiwa unanitegemea Mimi wakati unapokuwa katika uwepo Wangu na ikiwa unanitegemea Mimi kwa ujasiri. Lazima ubaki karibu na Mimi daima na kuweka mambo yote katika mikono Yangu. Usirudi nyuma. Baada ya kuwa karibu na Mimi kwa kipindi cha muda bila kujua, nia Zangu zitafichuliwa kwako. Ikiwa utazielewa, basi kweli utakuwa uso kwa uso na Mimi, na utakuwa umeupata uso wangu kweli. Utakuwa dhahiri na imara ndani na utakuwa na kitu cha kutegemea, na utakuwa na nguvu na ujasiri pia. Pia utakuwa na njia ya kusonga mbele na kila kitu kitakuja kwako kwa urahisi.

Sura ya 10

Haupaswi kuwa na hofu ya hili na lile. Haidhuru wingi wa matatizo na hatari unazokabili, utabaki thabiti mbele Yangu; usizuiliwe na kitu chochote, ili mapenzi Yangu yaweze kufanyika. Huu utakuwa ni wajibu wako, vinginevyo utakabiliana na ghadhabu Yangu na mkono wangu uta..., na utavumilia mateso ya akili yasio na mwisho. Ni lazima uyavumilie yote; kwa ajili Yangu, lazima uwe tayari kuviachilia vitu vyote unavyomiliki na kufanya kila kitu unachoweza kunifuata Mimi, na uwe tayari kutumia kila kitu chako. Sasa ndio wakati ambao Nitakujaribu: Je, utanipa uaminifu wako? Je, unaweza kunifuata Mimi hadi mwisho wa barabara kwa uaminifu? Usiwe na hofu; kwa msaada Wangu, ni nani angeweza daima kuzuia barabara? Kumbuka hiki! Kumbuka! Kila kitu ambacho hutokea ni kwa kusudi Langu njema na yote yako chini ya uangalifu Wangu. Je, kila neno na tendo lako linaweza kufuata neno Langu? Wakati majaribio ya moto yatakuja juu yako, utapiga magoti na kuomba msaada? Au wewe utajikunyata, bila uwezo wa kusonga mbele?

Lazima uwe na ushujaa Wangu ndani yako na lazima uwe na kanuni wakati unakabiliana na ndugu wasioamini. Lakini kwa ajili Yangu, si lazima pia usikubali kushindwa na nguvu zozote za giza. Tegemea hekima Yangu ili kutembea kwa njia kamili; usiruhusu njama za Shetani kuchukua umiliki. Weka juhudi zako zote katika kuuweka moyo wako mbele Zangu, nami Nitakufariji na kukuletea amani na furaha. Usijitahidi kuwa namna fulani mbele ya watu wengine; Je, si kunifanya Mimi niridhike kuna thamani na uzito zaidi? Kwa kuniridhisha, si utajazwa na amani na furaha ya milele hata zaidi? Mateso yako ya sasa yanaonyesha jinsi baraka zako za baadaye zitakavyokuwa; ni zizisoelezeka. Wewe hujui ukubwa wa baraka ambazo utapata; huwezi hata kuziota. Leo zakuwa halisi, halisi kweli! Hii haiko mbali sana, unaweza kuiona? Kila chemba ya mwisho ya hii iko ndani Yangu na ni jinsi gani kuna ung'avu mbele! Futa machozi yako, na usihisi uchungu au huzuni tena. Vitu vyote vimepangwa na mikono Yangu, na lengo Langu ni kuwafanya ninyi muwe washindi na kuwaleta katika utukufu pamoja na Mimi. Kwa yote yanayokutendekea, unapaswa kushukuru sawasawa na uwe uliyejawa na sifa; hilo litanifanya Niridhike sana.

Maisha ya kuzidi uwezo wa binadamu ya Kristo tayari imeonekana; hakuna kitu chochote unachopaswa kuhofia. Mashetani wako chini ya miguu yetu, na wakati wao hautakuwepo kwa muda muda mrefu zaidi. Amka! Tupilia mbali ulimwengu wa uasherati; jinusu mwenyewe kutoka dimbwi la kifo! Kuwa mwaminifu Kwangu bila kujali chochote, na usonge mbele kwa ujasiri; Mimi ni mwamba wako wa nguvu, kwa hivyo Nitegemee Mimi!

Sura ya 11

Je, Mimi ni Mungu wako? Je, Mimi ni Mfalme wako? Je, kweli umeniruhusu Mimi kutawala kama Mfalme ndani yako? Unapaswa kutafakari kujihusu kabisa. Je, hukuchunguza na kukataa mwanga mpya na hata kuthubutu kuacha bila kuufuata ulipokuwa ukija? Kwa sababu ya hili utapitia hukumu na kuanguka hadi kifo chako, utahukumiwa na kutandikwa kiboko na kiboko cha chuma na hutahisi kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa haraka utalia na kupiga magoti katika ibada wakati huo ukiomboleza. Nimewaambia daima na daima Nimewaeleza na Nimewaambia kila kitu. Fikirieni nyuma kulihusu kwa makini, ni wakati upi Nimewahi kukosa kuwaambia kitu? Hata hivyo, kuna watu fulani ambao wanashikilia kufanya mambo kwa njia ambayo si sahihi. Wamepotea katika ukungu wa shaka ambao unazuia jua na kamwe hawauoni mwanga. Je, hii si kwa sababu dhamira yao ya “nafsi” ni yenye nguvu sana ama mawazo yao wenyewe ni makubwa sana? Tangu lini wewe ukanifikiria Mimi? Tangu lini ukawa na nafasi kwa ajili Yangu katika moyo wako? Wakati umefeli, wakati huna uwezo, na wakati umeishiwa na uchaguzi, hapo tu ndipo unaomba Kwangu. Basi, mbona usifanye mambo wewe mwenyewe sasa? Enyi watu! Ni nafsi zenu nzee ambazo zimewaharibu!

Watu wengine hawawezi kupata njia, na hawawezi kufuata mwanga mpya. Wanashiriki tu kuhusu kile ambacho wameona awali, hakuna kitu kipya kwao. Mbona hivyo? Mnaishi ndani yenu na mmeniacha Mimi nje ya mlango. Unapoonza mbinu za kazi ya Roho Mtakatifu zikibadilika, moyoni mwako, daima wewe huwa mwangelifu kuhusu kuwa mwenye makosa. uchaji wako kwa Mungu uko wapi? Je, umelitafuta katika ukimya wa uwepo wa Mungu? Unatafakari tu: “Je, Roho Mtakatifu kweli anafanya kazi hivyo?” Watu wengine wameshuhudia kwamba ni kazi ya Roho Mtakatifu, lakini bado wana mambo kusema kuihusu. Watu wengine wanakiri kwamba ni neno la Mungu, lakini hawalikubali. Dhana tofauti zinafurika kuhusu kila mmoja wao, na hawaelewi kazi ya Roho Mtakatifu, wakiwa wazembe na wa ovyoovyo, bila hiari ya kulipa gharama na kuwa wenye bidii katika uwepo Wangu. Roho Mtakatifu amewapa nuru, lakini hawatakuja mbele Yangu kuwasiliana kwa karibu na kunitafuta. Badala yake, wanafuata tamaa zao wenyewe, wakifanya chochote wapendacho; ni nini nia yao?

Sura ya 12

Ikiwa una tabia ambayo si thabiti, nyepesi kuhamaki kama upepo au mvua, kama huwezi kuendelea kusonga mbele, basi fimbo Yangu haitakuwa mbali na wewe. Unaposhughulikiwa, kadiri hali ilivyo mbaya zaidi, na kadiri unavyoteswa zaidi, ndivyo upendo wako kwa Mungu unavyoongezeka, na unaacha kushikilia dunia. Bila njia nyingine, unakuja Kwangu, na unapata tena nguvu na imani yako. Ilhali, katika hali rahisi, ungeboronga. Ni lazima uingie ndani kwa mtazamo chanya, uwe mwenye vitendo na si baridi. Hutatingisika na yeyote na chochote katika hali yoyote, na huwezi kushawishiwa na maneno ya yeyote. Ni lazima uwe na tabia thabiti, na

bila kujali kile watu wanachoweza kusema, utatenda kile unachojua kuwa ukweli mara moja. Lazima daima uwe na maneno Yangu yakifanya kazi ndani yako, bila kujali ni nani unayemkabili; lazima uweze kusimama imara katika ushuhuda wako Kwangu na ufikirie mizigo Yangu. Hupaswi kuchanganyikiwa, ukikubaliana na watu bila kufikiri na bila kuwa na mawazo yako mwenyewe, ila badala yake lazima uwe na ujasiri wa kusimama na kupinga vitu visivyotoka Kwangu. Ukijua kwa dhahiri kwamba jambo si sahihi, ilhali unyamaze, basi wewe si mtu anayetenda ukweli. Ukijua kwamba jambo si sahihi na kisha ugeuze mada, lakini Shetani azuie njia yako—unazungumza bila athari yoyote na huwezi kuvumilia hadi mwisho—basi bado unabeba woga moyoni mwako, na moyo wako bado haujazwi na fikira kutoka kwa Shetani?

Mshindi ni nini? Wanajeshi wazuri wa Kristo lazima wawe jasiri na kunitegemea kuwa wenye nguvu kiroho; lazima wapigane kuwa wapiganaji na wapambane na Shetani hadi kufa. Lazima daima ukae macho, na hii ndiyo maana Nakuomba ushirikiane kwa vitendo na Mimi kila wakati na kujifunza kuja karibu nami. Ikiwa katika wakati wowote na katika hali yoyote, unaweza kubaki kimya mbele Yangu, ukisikiza usemi Wangu na kuzingatia maneno Yangu na matendo, basi hutashawishiwa na kupoteza msimamo wako. Chochote unachopata kutoka ndani Yangu kinaweza kutendwa. Kila neno Langu linaelekezwa kwa hali yako. Yanachoma moyo wako, na hata ukiyakana na kinywa chako, huwezi kuyakana na moyo wako, na ukichunguza maneno Yangu, utahukumiwa. Kwa maneno mengine, maneno Yangu ni ukweli, uhai, njia; hayo ni upanga mkali, ukatao kuwili na yanaweza kumshinda Shetani. Wale wanaoelewa na wana njia ya kutenda maneno Yangu wamebarikiwa, na wale wasioyatenda watahukumiwa pasipo shaka; hili ni jambo la busara sana. Sasa, kadiri ya wale Ninaowahukumu imepanuka. Sitahukumu tu mbele Yangu wale wanaonijua, ila wale wasioniamini na wanaojaribu kadiri wawezavyo kupinga na kuzuia kazi ya Roho Mtakatifu pia watahukumiwa. Wale wote wanaofuata nyayo Zangu mbele Yangu wataona kwamba Mungu ni moto mkali sana! Mungu ni uadhama! Anafanya hukumu Yake, na kuwahukumu kifo. Wale walio kanisani wasiozingatia kufuata kazi ya Roho Mtakatifu, wanaoingilia kazi ya Roho Mtakatifu, wanaojionyesha, walio na nia na malengo yasiyo sahihi, wasioweka jitihada yao katika kula na kunywa maneno ya Mungu, waliokanganyikiwa na wenye shaka, wanaochunguza kazi ya Roho Mtakatifu—maneno ya hukumu yatawajia wakati wowote. Matendo yote ya watu yatafichuliwa. Roho Mtakatifu huchunguza vina vya mioyo ya watu, hivyo usiwe asiyejali; kuwa mwangalifu na utahadhari, usitende bila kufikiri wewe binafsi. Ikiwa matendo yako hayafuati maneno Yangu, basi utahukumiwa. Hakuna haja ya kuiga, ya kuwa mwenye kujifanya, au ya kutoelewa kweli; lazima uje mbele Yangu na kuwasiliana kwa karibu na Mimi mara nyingi.

Chochote utakachochukua kutoka ndani Yangu, kitakupa njia ya kutenda, na utaandamana na nguvu Zangu, utakuwa na uwepo Wangu, na daima utembe katika maneno Yangu, utazidi

kila kitu duniani, na kuwa na nguvu ya ufufuo. Ikiwa maneno yako, tabia yako na matendo yako hayana maneno Yangu na uwepo Wangu, ukijitenga kutoka Kwangu na kuishi ndani yako, uishi katika dhana za akili, uishi katika mafundisho na amri, basi hiyo ni ithibati kwamba umeweka akili yako kwa dhambi. Kwa maneno mengine, unaendelea kushikilia nafsi yako nzee na huachi wengine wadhuru nafsi yako kidogo au kuharibu nafsi yako; mtu kama huyu ana ubora duni sana wa tabia na ni mpuuzi sana, na hawezi kuona neema ya Mungu au kutambua baraka za Mungu. Utaweza kuacha Nifanye kazi ndani yako lini ukiendelea kunikwepa! Wakati Nimemaliza kuzungumza, unasikiza lakini hukumbuki, na unakuwa mnyonge hasa shida zako zinapoonyeshwa kweli; hiki ni kimo cha aina gani! Ninaweza kukufanya uwe kamili lini ikiwa daima unahitaji kubembelezwa! Ikiwa unaogopa uvimbe na mikwaruzo, basi unapaswa kuharakisha kuwaonya wengine, “Sitamwacha yeyote anishughulikie, ninaweza kuondoa tabia yangu ya asili na nzee mimi mwenyewe.” Hivyo hakuna mtu atakukosoa au kukugusa, na uko huru kuamini njia yoyote unayotaka bila mtu yeyote kukujali. Je, unaweza kufuata nyayo Zangu hivi? Ni maneno matupu kusema kwamba una hakika kwamba mimi ni Mungu wako na Bwana wako. Ikiwa kweli huna shaka, mambo haya hayatakuwa shida, na utaamini kwamba ni upendo wa Mungu na baraka za Mungu juu yako. Ninapozungumza, ni kwa wana Wangu, na inapaswa kukabiliwa na shukrani na sifa.

Sura ya 13

Katika hali yenu ya sasa nyinyi hushika dhana za nafsi zaidi kupindukia, na madakizo yenu ya dini ni mazito kiasi. Mmeshindwa kutenda katika roho, hamwezi kufahamu kazi ya Roho Mtakatifu, na mmekataa mwanga mpya. Huoni jua wakati wa mchana kwa sababu wewe ni kipofu. Huwaelewi watu, umeshindwa kuwaacha “wazazi” wako, umekosa utambuzi wa kiroho, huijui kazi ya Roho Mtakatifu, na huna wazo la jinsi ya kula na kunywa ya neno Langu. Ni tatizo kuwa hujui jinsi ya kula na kunywa peke yako. Kazi ya Roho Mtakatifu hupiga hatua siku baada ya siku kwa kasi ya kushangaza. Kuna mwanga mpya kila siku, na kuna mambo mapya na safi kila siku, lakini huelewi. Badala yake, unapenda kufanya utafiti, na wewe huangalia mambo kupitia lenzi ya mapendeleo yako ya kibinafsi bila kuyazingatia kwa makini na husikiliza kwa bumbuwazi. Huombi kwa bidii katika roho, wala hunitazami au kutafakari zaidi juu ya maneno Yangu. Hivyo, yote uliyo nayo ni elimu, sheria na mafundisho. Lazima ujue jinsi ya kula na kunywa kutoka kwa neno Langu na kuja mbele Yangu daima na neno Langu.

Watu siku hizi hawawezi kukubali kujiachilia wenyewe, wao siku zote hufikiri kwamba wao ndio sahihi. Wao wamekwama katika dunia yao wenyewe ndogo na hawawi watu sahihi. Wakiendelea kusisitiza kuwa na lengo lisilo sahihi basi hakika watahukumiwa, na kama ni mbaya basi wataondolewa. Lazima uweke juhudi zaidi katika kuwa na ushirika wa kudumu na

Mimi na si kuwa na ushirika tu na yeyote umtakaye. Lazima uwe na ufahamu wa watu ambao huwa na ushirika nao na ushirika kuhusu masuala ya kiroho katika maisha, ni hapo tu unapoweza kuruzuku maisha kwa wengine na kufidia mapungufu yao. Hupaswi kuchukua sauti ya kuhubiri nao, ambao kimsingi ni msimamo mbaya kuwa nao. Katika ushirika ni lazima uwe na ufahamu wa mambo ya kiroho. Lazima uwe na hekima na kuwa na uwezo wa kuelewa ni nini kilicho katika mioyo ya watu wengine. Lazima uwe mtu mwafaka kama utawatumikia wengine na lazima ufanye ushirika na kile ulicho nacho.

Jambo la muhimu sasa ni kwako wewe kuwa na uwezo wa kufanya ushirika Nami, kuwasiliana kwa karibu Nami, kula na kunywa peke yako, na kuwa karibu na Mungu. Lazima uelewe haraka mambo ya kiroho na kuwa na uwezo wa kuona kwa njia ya mazingira na mambo yaliyopangwa katika eneo lako. Je, unaweza kuelewa kile Nilicho? Ni muhimu kwamba ule na kunywa kutegemea na kile unachokosa, na kuishi kwa kutegemea neno Langu! Tambua mikono Yangu, na wala usilalamike. Ukifanya hivyo na kujitenga, unaweza kupoteza nafasi ya kupokea neema ya Mungu. Anza kwa kunikaribia Mimi: Je, unakosa nini, unapaswa kunikaribia Mimi na kuuelewa moyo Wangu vipi? Ni vigumu kwa watu kuja karibu na Mimi kwa sababu hawawezi kuiachilia nafsi. Tabia yao daima haiwiani, kuwa moto na kisha baridi, na wao wanajivuna na kuridhika na wao wenyewe wanapopata ladha kidogo ya utamu. Baadhi ya watu bado hawajaamka, ni kiasi gani cha unayoyasema kina kile ulicho? Ni kiasi gani cha hayo ambacho ni kujitetea mwenyewe, au kuiga wengine ama tu kufuata kanuni? Sababu ya wewe kutofahamu au kuelewa kazi ya Roho Mtakatifu ni kuwa hujui jinsi ya kuwa karibu na Mimi. Kwa nje daima wewe hutafakari juu ya mambo, kutegemea dhana za nafsi na mawazo yako; wewe kwa siri hutafiti na kushiriki katika baadhi ya mipango midogo midogo, na huwezi hata kulileta hilo peupe. Hii inaonyesha kwamba kwa hakika huielewi kazi ya Roho Mtakatifu. Kama kwa hakika unaelewa kwamba jambo halitoki kwa Mungu, kwa nini usithubutu kusimama na kulikataa? Ni wangapi wangeweza kusimama na kuzungumza kwa ajili Yangu? Huonyeshi ujasiri wowote wa mtoto wa kiume.

Kila kitu ambacho kimepangwa sasa ni kwa lengo la kutoa mafunzo kwenu ili kwamba mkue katika maisha yenu, kuzifanya roho zenu ziwe na makali na zenye ncha, kuyafungua macho yenu ya kiroho na kuwafanya mtambue mambo yanayotoka kwa Mungu. Kitokacho kwa Mungu hukuwezesha kuhudumu kwa uwezo na mzigo na kuwa imara katika roho. Mambo ambayo hayatoki Kwangu yote ni matupu; hayakupi kitu, husababisha utupu katika roho yako na kukufanya upoteze imani yako, na kuweka umbali kati yako na Mimi, yakikufanya ufungiwe katika akili yako mwenyewe. Sasa unaweza kuvuka mipaka ya kila kitu katika ulimwengu wa kawaida unapoishi katika roho, lakini kuishi katika mawazo yako ni kuchukuliwa na Shetani na huu ni mwisho wa njia. Ni rahisi sana sasa: Nitegemee Mimi kwa moyo wako na roho yako mara

moja itakuwa imara, utakuwa na njia ya kutenda na Mimi nitakuongoza katika kila hatua. Neno Langu litafichuliwa kwako wakati wote na katika maeneo yote. Bila kujali ni wapi au wakati upi, au mazingira yako ni mabaya namna gani, Mimi nitakuonyesha kwa uwazi na moyo Wangu kufichuliwa kwako ukinitegemea Mimi kwa moyo wako; kwa njia hii utaikimbilia barabara iliyo mbele bila kupoteza njia. Baadhi ya watu hujaribu kupapasa kwa nje, lakini kamwe hawafanyi hivyo kutoka ndani ya roho zao. Mara nyingi hawawezi kuifahamu kazi ya Roho Mtakatifu. Wanapofanya ushirika na watu wengine, wao huchanganyikiwa zaidi, wakikosa njia ya kufuata na kutojua kitu cha kufanya. Watu hawa hawajui kinachowasumbua; wanaweza kuwa na mambo mengi na wawe wamejazwa sana ndani, lakini hilo lina maana yoyote? Je, kweli una njia ya kufuata? Je, umeangaziwa na kunurishwa? Je, una umaizi wowote mpya? Je, umefanya maendeleo au umerudi nyuma? Je, unaweza kujiendeleza na mwanga mpya? Huna utii; utii unaousema mara nyingi si kitu ila maongezi tu. Umeishi kwa kudhihirisha maisha ya utiifu?

Kikwazo cha mtu kujidai, kuridhika, majisifu, na kiburi ni kikubwa jinsi gani? Ni nani wa kulaumiwa usipoweza kuingia katika uhalisi? Lazima ujichunguze mwenyewe kwa makini ili kuona kama wewe ni mtu sahihi. Je, malengo yako hufanywa Nami katika mawazo? Je, maneno na matendo yako husimama mbele Yangu? Mimi huchunguza fikira na mawazo yako yote. Je, si unajihisi mwenye hatia? Unajitwika sura ya bandia ili wengine waone na wewe kwa upole unajifanya kujidai; hili hufanyika ili ujikinge mwenyewe. Wewe hufanya hili ili kuyaficha maovu yako, na hata kutafuta njia za kuusukuma huo uovu kwa mtu mwingine. Ni hila gani hukaa ndani ya moyo wako! Fikiria kila kitu ambacho umesema; haikuwa kwa faida yako kwamba ulikuwa na hofu kwamba roho yako mwenyewe ingepata madhara na hivyo ukamsitiri Shetani na kisha kuwaibia ndugu zako ulaji na unywaji wao kwa nguvu? Una nini la kusema juu yako mwenyewe? Je, unafikiri kwamba wakati mwingine utaweza kulipia kula na kunywa huko ambako Shetani amechukua wakati huu? Hivyo unaona wazi sasa, hiki ni kitu ambacho unaweza kufidia? Je, unaweza kuufidia wakati uliopotea? Lazima kwa bidii mchunguze wenyewe kuona ni kwa nini hapakuwa na kula na kunywa katika mikutano michache iliyopita na ni akina nani ambao walisababisha shida hii. Lazima mfanye ushirika mmoja kwa mmoja mpaka iwe wazi. Watu kama hawa wasipozuiwa bila huruma, akina ndugu hawataelewa, na basi itakuja kutokea tena tu. Macho yenu ya kiroho hayajafunguliwa na wengi wenu sana ni vipofu! Na wale ambao huona ni wa kutojali kuhusu hilo. Hawasimami na kuongea, nao, pia, ni vipofu. Wale ambao huona lakini hawaongei ni mabubu. Kuna wengi hapa ambao wana upungufu.

Baadhi ya watu hawaelewi ukweli ni nini, ni nini maisha, njia ni nini, na wao hawaelewi roho. Wao huangalia neno langu kama fomyula tu, na hili ni gumu mno kubadilika. Hawaelewi shukrani ya kweli na sifa ni nini. Baadhi ya watu hawawezi kufahamu mambo muhimu na ya msingi, badala yake, wao hufahamu tu ya upili. Inamaanisha nini kudakiza usimamizi wa

Mungu? Inamaanisha nini kubomoa jengo la kanisa? Inamaanisha nini kudakiza kazi ya Roho Mtakatifu? Kikaragosi wa Shetani ni nini? Ukweli huu lazima ueleweke wazi na sio tu kusitiriwa kwa mashaka. Ni kwa nini hakukuwa na kula na kunywa wakati huu? Baadhi ya watu wanaona kuwa wao wanapaswa kumsifu Mungu kwa sauti kubwa leo, lakini ni kwa jinsi gani wamsifu Yeye? Je, wanapaswa kuimba nyimbo na kucheza ngoma ili kumsifu Yeye? Je, njia nyingine hazihesabiki kama sifa? Baadhi ya watu huja kwa mikutano na dhana kwamba sifa za shangwe ndiyo njia ya kumsifu Mungu. Watu wana dhana hizi, na hawatilii maanani kazi ya Roho Mtakatifu, matokeo yake yakiwa kuwa bado kuna madakizo. Hakukuwa na kula na kunywa katika mkutano huu; wote wamesema kwamba wangeweza kuudhukuru mzigo wa Mungu na kutetea ushuhuda wa kanisa. Ni nani ambaye kweli amefikiri kwa makini kuhusu mzigo wa Mungu? Jiulize: Je, wewe ni mtu ambaye ameonyesha nadhari kwa mzigo wa Mungu? Je, unaweza kutenda haki kwa ajili ya Mungu? Je, unaweza kusimama na kuzungumza kwa ajili Yangu? Je, unaweza bila kusita kuweka ukweli katika vitendo? Je, wewe ni jasiri vya kutosha kupambana dhidi ya matendo yote ya Shetani? Je, unaweza kuwa na uwezo wa kuweka hisia zako kando na kufichua Shetani kwa sababu ya ukweli Wangu? Je, unaweza kuyaruhusu mapenzi Yangu yatimizwe ndani yako? Je, umejitolea moyo wako wakati muhimu unapowadia? Je, wewe ni mtu ambaye hufanya mapenzi Yangu? Jiulize na kufikiri juu yake mara kwa mara. Zawadi za shetani zimo ndani yako na wewe ni wa kulaumiwa kwa hayo kwa kuwa huwaelewi watu na umeshindwa kuitambua sumu ya Shetani; unajiongoza mwenyewe kwa kifo. Shetani amekudanganya kabisa kiasi kwamba umekanganyika kabisa; umelewa kwa divai ya uasherati na unayumba mbele na nyuma bila uwezo wa kushikilia maoni dhabiti na bila njia ya kutenda. Huli na kunywa vizuri, wewe hupigana na kugombana ovyo ovyo, hujui mema na mabaya na humfuata yeyote aongozaye—je, una ukweli wowote? Baadhi ya watu hujitetea hata kushiriki katika udanganyifu, wao hufanya ushirika na wengine lakini hilo huwaongoza hadi mwisho wa njia. Je, ni kutoka Kwangu ambapo watu hawa hupata nia zao, malengo, motisha, na chanzo? Je, unafikiri kuwa unaweza kufidia ndugu hawa kwa kula na kunywa kwao kulikochukuliwa? Tafuta watu wachache ili kufanya nao na kuwauliza, na uwaache wajizungumzie wenyewe: Je, wao wamepewa kitu chochote? Au wamekunywa na kuyajaza matumbo na maji machafu na kujawa na takataka na sasa hawana njia ya kufuata? Je, si hilo litabomoa kanisa? Upendo uko wapi kati ya ndugu? Kwa siri, wewe unatafiti ni nani aliye sahihi na asiye sahihi, lakini kwa nini huubebi mzigo kwa ajili ya kanisa? Kwa kawaida wewe hufanya vizuri katika kupiga ukelele wa misemo, lakini mambo yanapotokea katika hali halisi wewe ni una mashaka kuyahusu. Baadhi ya watu huelewa lakini hunung'unika tu kimya kimya wakati wengine huongea yale wanayoyaelewa lakini hakuna mtu mwingine husema neno. Wao hawajui kinachotoka kwa Mungu na ni nini kazi ya Shetani. Ziko wapi hisia zenu za ndani kuhusu maisha? Kabisa hamuifahamu kazi ya Roho Mtakatifu na hamuitambui kazi ya Roho Mtakatifu na ni vigumu kwenu kukubali mambo mapya.

Nyinyi hukubali tu mambo ya kidini na ya kidunia, ambayo hupatana na dhana za watu. Kwa hivyo, nyinyi hupambana kitundu. Ni wangapi wanaweza kufahamu kazi ya Roho Mtakatifu? Ni wangapi ambao kwa hakika wamebeba mzigo kwa ajili ya kanisa? Je, unaufahamu? Kuimba nyimbo ni njia moja ya kumsifu Mungu, lakini huelewi kwa dhahiri ukweli wa kumsifu Mungu na wewe ni mgumu katika njia unayoitumia kumsifu Yeye. Si hilo ni wazo lako mwenyewe? Daima wewe hushika dhana zako mwenyewe bila kuachilia na huwezi kuzingatia kile Roho Mtakatifu atakachofanya leo, usiweze kuhisi yale ndugu zako wanahisi, na kushindwa kutafuta mapenzi ya Mungu kwa njia ya utulivu. Wewe hufanya mambo kwa upofu na kuimba nyimbo vyema, lakini matokeo yake ni machafuko kamili. Je, hiyo kweli ni kula na kunywa? Je, unaona ni nani hasa anayesababisha madakizo? Kimsingi wewe huishi katika roho, lakini badala yake hushikilia dhana mbalimbali—Hiyo kwa vyovyote vile, inawezaje kuwa kulibeeba kanisa mzigo? Lazima muone kwamba kazi ya Roho Mtakatifu inaendelea hata kwa kasi zaidi sasa, kwa hivyo si nyinyi mnakuwa vipofu kama mnashikilia kikiki dhana zenu wenyewe na kupinga kazi ya Roho Mtakatifu? Si hilo ni kama nzi kuruka akigonga kuta na kuvuma pote? Mkiendelea kwa njia hii mtatupwa kando.

Wale ambao wamefanywa kuwa kamili kabla ya maafa ni watiifu kwa Mungu. Wao huishi wakimtegemea Kristo, humshuhudia Kristo, na humtukuza Yeye. Wao ni watoto wa kiume waliofanikiwa na askari wema wa Kristo. Ni muhimu sasa kwamba ujitulize mwenyewe na kuja karibu na Mungu na kufanya ushirika Naye. Kama huwezi kuja karibu na Mungu, una hatari ya kutekwa na Shetani. Kama unaweza kuja karibu na Mimi na kufanya ushirika na Mimi, ukweli wote utafichuliwa kwako, na wewe utakuwa na kiwango cha kufuata kwa maisha yako na vitendo. Kwa sababu wewe ni mmoja ambaye yu karibu na Mimi, neno Langu kamwe halitaondoka kando yako, na hutapotea kutoka kwa neno Langu katika maisha yako; Shetani hatakuwa na njia ya kukudanganya, na badala yake ataona aibu na kutoroka kwa kushindwa. Ukitafuta nje kile kinachokosa ndani yako, kunaweza kuwa na nyakati ambapo unapata baadhi yacho, lakini sehemu kubwa yacho itakuwa sheria na kinaweza kuwa kitu usichohitaji. Lazima ujiachilie mwenyewe na ule na kunywa kutoka kwa neno Langu zaidi na ujue jinsi ya kulitafakari neno Langu. Kama huelewi kitu, njoo karibu Nami na kufanya ushirika na Mimi mara nyingi; kwa njia hii, kile utakachokielewa kitakuwa halisi na cha kweli. Lazima uanze kwa kuwa karibu Nami. Hili ni muhimu! Vinginevyo, hutajua jinsi ya kula na kunywa. Huwezi kula na kunywa wewe mwenyewe—kimo chako kweli ni kidogo mno.

Sura ya 14

Hapana muda wa kupoteza sasa. Roho Mtakatifu hutumia njia nyingi tofauti za kutuongoza katika maneno ya Mungu. Unapaswa kujitayarisha na ukweli wote, kutakaswa, kuwa na undani

wa kweli na ushirikiano na Mimi; huruhusiwi nafasi yoyote ya kuchagua. Kazi ya Roho Mtakatifu haina hisia na haijali wewe ni mtu wa aina gani. Mradi tu wewe uko tayari kutafuta na kufuata—si kutoa visingizio, si kubishana juu ya mafanikio yako mwenyewe na hasara lakini kutafuta na njaa na kiu ya haki, basi Nitakupa nuru. Bila kujali jinsi ulivyo mpumbavu na mjinga, Mimi sioni vitu kama hivyo. Naangalia kuona jinsi unavyofanya kazi kwa bidii katika hali ya kujenga. Kama bado unashikilia dhana ya nafsi, kuzungusha duara katika dunia yako ndogo, basi Nafikiri uko katika hatari.... kuchukuliwa kuenda mbinguni ni nini? Inamaanisha nini kutelekezwa? Unapaswa kuishi vipi mbele ya Mungu leo? Unapaswa kushirikiana kikamilifu Nami vipi? Zitupilie mbali dhana zako mwenyewe, jichanganue mwenyewe, ivue barakoa yako, ona dhahiri ubainifu wa tabia yako halisi, jichukie mwenyewe, kuwa na moyo unaotafuta kwa njaa na kiu ya haki, amini kwamba wewe mwenyewe kwa kweli si kitu, kuwa tayari kujiachilia mwenyewe, kuwa na uwezo wa kuacha njia zako zote za kufanya mambo, jitulize mwenyewe mbele Yangu, yafanye maombi zaidi, jiegemeze Kwangu kwa unyofu, nitegemee Mimi, na usiache kuwa karibu na Mimi na kuwa na ushirika na Mimi—hili ni muhimu. Watu mara nyingi hujipata wamenaswa ndani ya nafsi zao wenyewe na hawako mbele ya Mungu.

Kazi ya sasa ya Roho Mtakatifu kwa kweli ni ngumu kwa watu kuwaza na yote huingia katika uhalisi; kwa kweli haitakufaa kuwa mzembe. Kama moyo wako na mawazo si sahihi, basi hutakuwa na njia. Kutoka mwanzo hadi mwisho ni lazima uwe macho wakati wote na kuhakikisha kuwa umejikinga dhidi ya uzembe. Heri wale ambao daima huwa macho na kusubiri na ambao wako kimya mbele Yangu! Heri wale ambao daima hunitegemea Mimi kwa mioyo yao, ambao huhakikisha wameisikiliza kwa karibu sauti Yangu, ambao huzingatia matendo Yangu na ambao huweka maneno Yangu katika matendo! Wakati kweli hauwezi kuvumilia taahira; mabaa ya kila namna yataenea, yakifungua midomo yao mikali, yenye damu kuwala nyinyi nyote kama mafuriko. Wanangu! Wakati umefika! Hakuna nafasi zaidi ya kuwaza. Njia pekee itakayowaleta chini ya ulinzi Wangu ni kurudi Kwangu. Ni lazima muwe na nguvu ya tabia ya mwana wa kiume, msiwe wadhaifu au kuvunjika moyo; lazima mfuate unyounyo hatua Zangu, msikatae mwanga mpya na, kwa kuwaambia jinsi ya kula na kunywa, mnapaswa mtii na kula na kunywa vizuri. Je, bado kuna wakati sasa wa kupigana au kushindana na kila mmoja kiholela? Je, mnaweza kufanya vita kama hamli na kushiba na hamjatayarishwa kikamilifu na ukweli? Kama mnataka kuishinda dini, ni lazima mjitayarishe kikamilifu na ukweli. Kuleni na kunywa maneno Yangu zaidi na kutafakari juu ya maneno Yangu zaidi. Lazima mle na kunywa maneno Yangu kwa kujitegemea na kuanza kwa kujongea karibu na Mungu. Acha hili liwe ni onyo kwenu! Lazima mtie maanani! Wale ambao ni werevu lazima kwa haraka waelewe ukweli! Achilia mambo yote ambayo huna nia ya kuyaacha. Nakwambia kwa mara nyingine tena

kwamba mambo haya kwa kweli ni hatari kwa maisha yako na yasiyokuwa na manufaa! Natumaini unaweza kunitegemea Mimi katika matendo yako, vinginevyo njia tu iliyo mbele itakuwa njia ya kifo, na ni wapi basi utakakokwenda kutafuta njia ya maisha? Uondoe moyo wako ambao unapenda kujishughulisha na mambo ya nje! Uondoe moyo wako ambao huwakaidi watu wengine! Kama maisha yako hayawezi kukomaa na umetelekezwa, si wewe basi utakuwa ndiye ambaye amejikwaa mwenyewe? Kazi ya Roho Mtakatifu sasa si kama wewe unavyofikiria. Kama huwezi kuziachilia dhana zako basi utapata hasara kubwa. Kama kazi ingekuwa ni kwa kuambatana na dhana za mtu, je, asili yako ya zamani na dhana zingeweza kufichuka? Je, ungeweza kuwa na uwezo wa kujijua mwenyewe? Labda bado unadhani kuwa huna dhana, lakini wakati huu bado pande zako zote mbalimbali mbaya zitafichuka. Kwa makini jiulize:

Je, wewe ni mtu ambaye hunitii Mimi?

Je, una hiari na tayari kuiachilia nafsi yako na unifuata Mimi?

Je, wewe ni mtu ambaye huutafuta uso Wangu kwa moyo safi?

Je, unajua jinsi ya kujongea karibu na Mimi na kufanya ushirika nami?

Je, unaweza kujituliza mbele Yangu na kutafuta mapenzi Yangu?

Je, wewe huweka katika vitendo maneno ambayo Mimi hukufichulia?

Je, unaweza kudumisha hali ya kawaida mbele Yangu?

Je, una uwezo wa kuona undani wa mipango ya hila ya Shetani? Je, wewe unathubutu kuifichua?

Ni jinsi gani unafanya busara kuhusu mzigo wa Mungu?

Je, wewe ni mtu ambaye hufanya busara kwa mzigo wa Mungu?

Je, wewe huielewaje kazi ya Roho Mtakatifu?

Je, ni jinsi gani wewe huhudumu kwa uratibu katika familia ya Mungu?

Je, wewe huwa na ushuhuda wa nguvu kwa ajili Yangu?

Je, wewe kupiganaje vita vizuri kwa ajili ya ukweli?

Lazima uchukue muda wa kutafakari ukweli huu kabisa. Ukweli ni wa kutosha kuthibitisha kuwa siku i karibu sana. Ni lazima ufanywe mkamilifu kabla ya maafa—hili ni suala la umuhimu

mkubwa ambalo lazima litatuliwe haraka! Nataka kuwafanya wakamilifu, lakini Naona kwamba nyinyi kweli kwa kiasi fulani hamjadhibitiwa. Mna ushupavu lakini hamuuweki kwa matumizi bora na bado hamjalewa mambo yaliyo muhimu zaidi, badala yake yote mnayoelewa ni mambo madogo. Kuna faida gani katika kujadili juu ya mambo haya? Je, si huku ni kupoteza wakati? Mimi huwaonyesha wema kwa njia hii lakini mnashindwa kuonyesha shukrani yoyote na nyinyi hupigana tu miongoni mwenu, hivyo si juhudi Zangu zote zimekuwa bure? Kama mtaendelea kwa njia hii, Sitachukua wakati kuwashawishi muendele! Nawaambia, isipokuwa mzinduke kwa ukweli, kazi ya Roho Mtakatifu itaondolewa kutoka kwenu! Hamtapewa cha kula zaidi tena, na mnaweza kuamini kama mnavyoona inafaa. Maneno Yangu yamesemwa kwa kirefu; msikilize au la, ni juu yenu. Wakati utakapofika mnapokuwa mmechanganyikiwa na hakuna njia ya kwenda mbele na hamuwezi kuona mwanga wa kweli, mtanilaumu Mimi? Ujinga ulioje! Matokeo yanapaswa kuwa yapi iwapo utajigandamia kikiki na kukataa kujiachilia? Si kazi yenu itakuwa ilikuwa zoezi la bure? Ni sikitiko lililoje kutupwa kando wakati janga linapokumba!

Sasa ni awamu muhimu ya ujenzi wa kanisa. Kama huwezi kushirikiana na Mimi kwa kupanga na kujitoa mwenyewe Kwangu kwa moyo wote, kama huwezi kuacha kila kitu, basi utapata hasara; bado unaweza kuwa na nia zingine? Mimi Niliwaonyesha huruma kwa njia hii, Nikiwasubiri mtubu na kuanza upya. Lakini wakati kweli hauruhusu hili sasa na ni lazima Nizingatie jambo lote zima. Kwa ajili ya madhumuni ya mpango wa usimamizi wa Mungu, kila kitu kinasonga mbele na hatua Zangu zapiga hatua siku kwa siku, saa kwa saa, wakati kwa wakati, na wale ambao hawawezi kuendelea sawa watatelekezwa. Kila siku kuna mwanga mpya, kila siku matendo mapya hufanyika, kuna mambo mapya kila siku na wale ambao hawawezi kuona mwanga ni vipofu! Wale ambao hawawezi kufuata wataondolewa....

Sura ya 15

Kuonekana kwa Mungu tayari kumetokea katika makanisa yote. Roho ndiye anayeongea, Yeye ni moto mkali, Yeye hubeba uadhama na Anahukumu; Yeye ni Mwana wa Adamu, aliyevaa vazi lililofika miguuni, na kufungwa mshipi kwenye matiti na ukanda wa dhahabu. Kichwa Chake na nywele Zake ni nyeupe kama sufu nyeupe, na macho Yake ni kama mwale wa moto; na miguu Yake iko kama shaba iliyosuguliwa sana, kana kwamba imesafishwa katika tanuru; na sauti Yake kama sauti ya maji mengi. Ana nyota saba katika mkono Wake wa kuume, upanga mkali wenye makali kuwili uko katika kinywa Chake na uso Wake ni kama jua liking'aa kwa nguvu zake!

Mwana wa Adamu Ameshuhudiwa, na Mungu Mwenyewe amefichuliwa waziwazi. Utukufu wa Mungu umekuja, uking'aa vikali kama jua lichomalo! Uso Wake mtukufu unawaka kwa mwanga ung'aao; ni macho ya nani yatathubutu kumtendea kwa upinzani? Upinzani

husababisha kifo! Hakuna hata chembe ya rehema kwa kitu chochote unachofikiri katika moyo wako, neno lolote usemalo au chochote ufanyacho. Nyinyi nyote mtakuja kuelewa na kuja kuona ni nini ambacho mmekipata—hakuna chochote ila hukumu Yangu! Naweza kukistahimili wakati nyinyi hamuweki juhudi zenu katika kula na kunywa maneno yangu, lakini hudakiza kiholela na kuharibu ujenzi Wangu? Mimi sitamhurumia mtu wa aina hii! Mengine makubwa zaidi na utaangamizwa katika moto! Mwenyezi Mungu hudhihirika katika mwili wa kiroho, bila hata chembe ya mwili au damu ikiunganisha mwili mzima. Yeye huvuka mipaka ya ulimwengu dunia, kama Ameketi kwenye kiti kitukufu cha enzi katika mbingu ya tatu, Akisimamia mambo yote! Ulimwengu na vitu vyote vimo mikononi Mwangu. Kama Nikisema, itakuwa. Kama Nikiliamua, ndivyo litakavyokuwa. Shetani yu chini ya miguu Yangu, yu katika kuzimu! Sauti Yangu itakapotoka, mbingu na nchi zitapita na kuwa bure! Mambo yote yatafanywa upya na huu ni ukweli wa kweli sana usiobadilika. Nimeushinda ulimwengu, kuwashinda waovu wote. Naketi hapa nikizungumza nanyi; wale wote ambao wana masikio wanapaswa kusikiliza na wale wote wanaoishi wanapaswa kukubali.

Siku zitafika mwisho; mambo yote katika dunia yatakuwa bure, na mambo yote yatazaliwa upya. Kumbuka hili! Kumbuka hili! Hapawezi kuwa na utata! Mbingu na nchi zitapita lakini maneno Yangu hayatapita! Acha Niwasihi kwa mara nyingine tena: Msikimbie bure! Amkeni! Tubuni na wokovu umekaribia! Tayari Nimeonekana miongoni mwenu na sauti Yangu imetokea. Sauti yangu imetokea mbele yenu, uso kwa uso na nyinyi kila siku, safi na mpya kila siku. Unaniona Mimi na Ninakuona wewe, Ninasema na wewe mara kwa mara, uso kwa uso na wewe. Na, bado unanikataa Mimi, hunijui Mimi; Kondoo Wangu wasikia sauti Yangu na bado mnasita! Mnasita! Mioyo yenu imepumbaa, macho yenu yamepofushwa na Shetani na hamuwezi kuuona uso Wangu mtukufu—ni kusikitisha kulikoje! Kusikitisha kulikoje!

Roho saba mbele ya kiti Changu cha enzi watumwa kwa kila pembe ya dunia na Mimi Nitamtuma Mjumbe Wangu kuzungumza kwa makanisa. Mimi ni mwenye haki na mwaminifu, Mimi ni Mungu achunguzaye sehemu ya ndani kabisa ya moyo wa mtu. Roho anaongea na makanisa na ni maneno Yangu yanayotiririka kutoka ndani ya Mwanangu; wale wote ambao wana masikio wanapaswa kusikiliza! Wale wote ambao wanaishi wanapaswa kukubali! Yaleni tu na kuyanywa, na msitilie shaka. Wale wote ambao huyatii na kuyasikiza maneno Yangu watapokea baraka kuu! Wale wote wautafutao uso Wangu kwa kweli watapata mwanga mpya kwa hakika, nuru mpya na ufahamu mpya; wote watakuwa wasafi na wapya. Maneno Yangu yataonekana kwako wakati wowote na yatafungua macho ya roho yako ili uweze kuona siri zote za ulimwengu wa kiroho na kwamba ufalme uko miongoni mwa binadamu. Ingia katika hifadhi na neema yote na baraka zitakuwa juu yako, njaa na baa hazitaweza kukugusa, mbwa mwitu, nyoka, chui wakubwa na chui hawataweza kukudhuru. Utaenda na Mimi, utembe na Mimi, na

uingie katika utukufu pamoja na Mimi!

Mwenyezi Mungu! Mwili Wake mtukufu waonekana wazi wazi, mwili mtakatifu wa kiroho watokea na Yeye ndiye Mungu Mwenyewe kamili! Dunia na mwili vyote vimegeuzwa na mabadiliko Yake juu ya mlima ambaye ni nafsi ya Mungu. Amevaa taji la dhahabu kichwani, mavazi Yake ni meupe kabisa, kifuani ana ukanda wa dhahabu na vitu vyote katika dunia ni mahali pa kuweka miguu yake. Macho Yake ni kama mwale wa moto, na upanga mkali wenye makali kuwili uko ndani ya kinywa Chake na Ana nyota saba katika mkono Wake wa kuume. Njia ya kwenda kwa ufalme ni ng’avu bila kikomo na utukufu Wake watokea na kuangaza; milima huwa na furaha na maji hucheka, jua, mwezi na nyota zote zazunguka kwa mpango wao wa taratibu, ukimkaribisha Mungu wa kweli na wa kipekee, ambaye kurudi kwake kwa ushindi kunaashiria ukamilisho wa miaka elfu sita ya mpango Wake wa usimamizi. Zote zaruka na kucheza kwa furaha! Shangilia! Mwenyezi Mungu amekaa juu ya kiti Chake kitukufu cha enzi! Imbeni! Bendera ya ushindi ya Mwenyezi inainuliwa juu ya mlima mwadhimu, mtukufu wa Sayuni! Mataifa yote yanashangilia, watu wote wa mataifa wanaimba, Mlima Sayuni unacheka kwa furaha, utukufu wa Mungu umetokea! Hata katika ndoto Sijawahi kufikiri kwamba Ningeuona uso wa Mungu lakini leo Nimeuona. Uso kwa uso na Yeye kila siku, nauweka wazi moyo wangu Kwake. Yeye kwa ukarimu hutoa vyote vinavyoliwa na kunywewa. Maisha, maneno, matendo, mawazo, nia—mwanga Wake mtukufu huwatia nuru wote. Yeye huongoza kila hatua ya njia, na kama moyo wowote ni muasi basi hukumu Yake itatokea mara moja.

Kula pamoja na Mungu, kukaa pamoja, kuishi pamoja, kuwa pamoja na Yeye, kutembea pamoja, kufurahia pamoja, kupata utukufu na baraka pamoja, kushiriki ufalme na Mungu, na kuwa pamoja katika ufalme—oo, ni furaha iliyoje! Oo, ni utamu ulioje! Uso kwa uso kila siku, kuzungumza kila siku, kuzungumza mara kwa mara, kupata nuru upya na ufahamu mpya kila siku. Macho yetu ya kiroho yanafunguliwa na tunaona kila kitu, siri zote za kiroho zinafichuliwa kwetu. Maisha matakatifu si ya kujali. Kimbia kwa haraka na usisite, songa mbele mfululizo, kuna maisha ya ajabu zaidi mbele. Usiridhike tu na ladha tamu lakini siku zote tafuta kuingia ndani ya Mungu. Yeye anajumuisha yote na mkarimu, na Ana kila aina ya vitu ambavyo tumekosa. Shirikiana kwa vitendo, ingia ndani Yake na hakuna kitu kitakachokuwa kama awali tena. Maisha yetu yatakuwa ya uvukaji mipaka na hakuna mtu, jambo, au kitu kitakachoweza kutuvuruga.

Uvukaji mipaka! Uvukaji mipaka! Uvukaji mipaka wa kweli! Maisha ya Mungu ya uvukaji mipaka yako karibu na vitu vyote kwa kweli vinakuwa na pumziko! Tunavuka mipaka ya dunia na mambo ya kidunia, hatuhisi upendo kwa waume au watoto. Tunavuka mipaka ya udhibiti wa ugonjwa na mazingira. Shetani hatothubutu kutuvuruga. Kuvuka kabisa mipaka ya maafa yote—

hii ni kumruhusu Mungu kuuchukua ufalme! Tunamkanyaga Shetani chini ya miguu, kuwa shahidi kwa ajili ya kanisa na kuifunua kikamilifu sura mbovu ya Shetani. Ujenzi wa kanisa u katika Kristo, mwili mtukufu umetokea—huku ni kuishi katika hali ya kuchukuliwa kuenda mbinguni!

Sura ya 16

Baada ya ushuhudiaji wa Mwana wa Adamu, Mwenyezi Mungu alijifichua kwetu hadharani kama Jua la haki. Haya ndiyo mabadiliko mlimani! Sasa inakuwa halisi zaidi na zaidi, na zaidi kuwa jambo la uhalisi. Tumeona utaratibu wa kazi ya Roho Mtakatifu, Mungu Mwenyewe ameibuka kutoka kwa mwili wa damu. Yeye hayuko chini ya udhibiti wa mwanadamu, wala anga, wala jiografia; Yeye huvuka mipaka ya nchi na bahari, Yeye hufika miisho halisi ya ulimwengu, na mataifa yote na watu wa jumua zote wanasikiliza sauti Yake kwa utulivu. Tunapofungua macho yetu ya kiroho tunaona kuwa neno la Mungu limetokea kwa mwili Wake mtukufu; ni Mungu Mwenyewe anayetokea kutoka kwa mwili. Yeye ni Mungu Mwenyewe halisi na kamili. Yeye husema nasi hadharani, Yeye yuko nasi uso kwa uso, Yeye hutushauri, Yeye hutuhurumia, Yeye hutusubiri, Yeye hutufariji, Yeye hutufundisha nidhamu na hutuhukumu. Yeye hutuongoza kwa mkono na utunzaji Wake kwetu huwasha kama ulimi wa moto ndani Yake, kwa moyo wa hamu Yeye hutuharakisha kuamka na kuingia ndani Yake. Maisha Yake yanayozidi uwezo wa binadamu yameguzishwa ndani yetu sote, na wote wanaoingia ndani Yake watafikia uvukaji mipaka na kuushinda ulimwengu na wale wote waovu, na kutawala pamoja naye. Mwenyezi Mungu ni mwili wa kiroho wa Mungu. Yeye akiliamua, ndivyo litakavyokuwa; Yeye akiliongea, litakuwa, na Yeye akiliamrisha, basi ndivyo; Yeye ndiye Mungu mmoja wa kweli! Shetani yuko chini ya miguu Yake, katika shimo la kuzimu. Kila kitu katika ulimwengu kimo mikononi Mwake; wakati umefika, na wote watarudi katika hali ya kutokuwepo na kuzaliwa upya.

Sura ya 17

Kanisa linajengwa na Shetani anajaribu kwa uwezo wake kulibomoa. Anataka kubomoa ujenzi Wangu kwa njia yoyote iwezekanayo, kwa hivyo, lazima kanisa litakaswe kwa haraka. Lazima kusiwe na makapi au mabaki yoyote maovu; lazima litakaswe ili lisiwe na dosari na libaki takatifu kama awali. Lazima muwe macho na kusubiri kila wakati, na ni lazima mje mbele Yangu zaidi. Lazima mtambue mipango ya njama na hila mbalimbali za Shetani, mjue roho, mjue watu na mweze kupambanua watu wa aina zote, masuala na mambo; lazima mle na mnywe maneno Yangu zaidi na, muhimu zaidi, lazima mweze kuyala na kuyanywa nyinyi wenyewe. Jiandaeni wenyewe na ukweli wote, njooni mbele Yangu ili nifungue macho yenu ya kiroho na kuwaruhusu kuona siri zote zilizo rohani.... Wakati kanisa linaingia awamu yake ya ujenzi,

watakatifu wanatembea wakienda vitani. Vipengele mbalimbali vya Shetani vya kutisha Vinawekwa mbele yenu; je, mnaacha na kurudi nyuma au mnainuka na kuendelea mkinitegemea Mimi? Weka hadharani vipengele vya Shetani vyenye upotovu na viovu, bila hisia wala huruma! Pambana na Shetani hadi kifo! Mimi ni msaada wenu na ni lazima muwe na roho ya mwana wa kiume! Shetani yuko katika hekaheka zake za kifo cha mwisho lakini bado hataweza kuhepa hukumu Yangu. Shetani yuko chini ya miguu Yangu na pia anakanyagwa chini ya miguu yenu— ni ukweli!

Wale wapinga dini wote na wale ambao hubomoa ujenzi wa kanisa hawafai kuvumiliwa hata kidogo na nitawahukumu mara moja. Weka Shetani hadharani, mkanyagie chini ya miguu, muangamize kabisa na usimuachie pa kujificha. Kila aina ya mapepo na vizuka hakika wataonyesha maumbile yao ya kweli mbele Yangu na Nitawatupa wote kuzimu ambamo hawatawahi kuwa huru; wote wako chini ya miguu yetu. Kama unataka kupigana vita vizuri kwa ajili ya ukweli, basi kwanza kabisa, usimpe Shetani nafasi ya kufanya kazi, na ili kufanya hivi mtastahili kuwa na nia moja na muweze kutumika katika kushirikiana, acheni dhana zenu za kibinafsi, maoni, mitazamo na njia za kufanya mambo, tuliza moyo wako ndani Yangu, zingatia sauti ya Roho Mtakatifu, kuwa makini na kazi ya Roho Mtakatifu na uwe na uzoefu wa maneno ya Mungu kwa kina. Lazima uwe na nia moja tu, ambayo ni kwamba mapenzi Yangu yaweze kufanyika. Hupaswi kuwa na nia nyingine. Lazima uangalie Kwangu kwa moyo wako wote, angalia hatua Zangu na Ninavyotenda mambo kwa karibu, na wala usiwe mzembe kabisa. Roho yako lazima iwe amilifu, macho yako yakiwa wazi. Kwa kawaida, wale ambao nia na malengo yao si sahihi, wale ambao wanapenda kuonekana na wengine, wenye hamu ya kutenda mambo, wenye tabia ya kukatiza, walio imara katika mafundisho ya dini, watumishi wa Shetani, nk., watu hawa wanapoinuka wanakuwa ugumu kwa kanisa na kula na kunywa kwa ndugu kunakuwa si kitu; unapompata mtu wa aina hii jifanye kisha mpige marufuku mara moja. Iwapo hawabadiliki licha ya maonyo ya kurudia, basi watapata hasara kubwa. Kama wale wanaoendelea katika njia zao kwa ukaidi wanajitetea na kujaribu kufunika dhambi zao, kanisa linapaswa kuwaondoa mara moja na kutowaachia nafasi ya kuendelea. Usipoteze mengi kwa kujaribu kuokoa machache, na uzingatie makubwa.

Macho yako ya kiroho lazima sasa yafunguke, na kutofautisha aina kadhaa za watu kanisani:

Je, ni mtu wa ina gani anaelewa masuala ya kiroho na anajua roho?

Je, ni mtu wa ina gani haelewi masuala ya kiroho?

Je, ni mtu wa ina gani ana roho waovu ndani yake?

Je, ni mtu wa ina gani ana Shetani anafanya kazi juu yake?

Je, ni mtu wa ina gani ambaye ana tabia ya kukatiza?

Je, ni mtu wa ina gani ambaye Roho Mtakatifu anatenda kazi kwake?

Je, ni mtu wa ina gani huonyesha kuzingatia kuelekea mzigo wa Mungu?

Je, ni mtu wa ina gani anaweza kufanya mapenzi Yangu?

Je, ni nani shahidi Wangu mwaminifu?

Jua ya kwamba nuru ambayo Roho mtakatifu hupatia makanisa yote ni maono ya leo ya juu zaidi. Msichanganyikiwe kuhusu mambo haya, lakini badala yake lazima mchukuwe muda wa kuyafikiria kabisa—hii ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya maisha yenu! Kama huelewi mambo haya yaliyo machoni pako basi hutakuwa na uwezo wa kusonga mbele, utakuwa katika hatari ya majaribu na ufungwa wakati wowote, na huenda ukavamiwa. Jambo kuu sasa ni kuzingatia kuweza kuwa karibu na Mimi moyoni mwako, kufanya ushirika zaidi na Mimi, na chochote unachokosa au kutafuta utafidiwa kupitia kuwa karibu na Mimi na kufanya ushirika na Mimi. Maisha yako hakika yatashughulikiwa na utakuwa na nuru mpya. Mimi kamwe siangalii jinsi mlikuwa wajinga awali na siyakumbuki makosa yenu. Mimi huangalia jinsi mnavyonipenda: Je, mnaweza kunipenda zaidi ya mambo mengine yote? Naangalia kuona iwapo mnaweza kugeuka nyuma na kunitegemea kuondoa ujinga wenu au la. Baadhi ya watu husimama Kwangu, kunipinga hadharani, na kuhukumu watu wengine; hawajui maneno Yangu, na hata uwezekano wao wa kuona uso Wangu uko chini. Wote wale walio mbele Yangu ambao hunifuata kwa dhati, ambao wana mioyo yenye njaa na kiu cha haki, Nitawapa nuru, kuwafichulia, kuwaruhusu kuniona kwa macho yenu na kugusa mapenzi Yangu wenyewe; hakika moyo Wangu utafichuliwa kwenu, ili mpate kuelewa. Lazima muweze kutenda yale ambayo naangaza ndani yenu kulingana na maneno Yangu, vinginevyo mtahukumiwa. Fuata mapenzi Yangu na hamtapotea.

Kwa wote wale wanaotafuta kuingia katika maneno Yangu, neema na baraka vitaongezeka mara dufu yao, watapata nuru na utambuzi mpya kila siku, na kujisikia wapya katika kula na kunywa kwa maneno Yangu kila siku. Watayaonja vinywani mwao wenyewe: Ni tamu jinsi gani! ... Lazima uwe makini, na usitosheke unapokuwa na ufahamu kiasi na ladha kiasi ya utamu—cha msingi ni kuendelea kutafuta mbele! Baadhi ya watu hufikiria ya kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ni kweli ajabu na halisi—huyu kweli ni nafsi ya Mwenyezi Mungu anafichuliwa wazi, na ishara na maajabu kubwa zaidi viko mbele. Kuwa makini na macho wakati wote, angalia kabisa kwenye chanzo, kuwa mtulivu mbele Yangu, zingatia na usikilize kwa makini, na

kuwa na uhakika kuhusu maneno Yangu. Haiwezekani kuwa na utata; kama una shaka hata kidogo basi Nina hofu kuwa utatupwa nje ya lango. Kuwa na maono wazi, simama kwenye sakafu ngumu, fuata mkondo huu wa maisha na uufuate popote ufikapo; usisite hata kidogo kabisa. Kula, kunywa na kutoa sifa tu, tafuta kwa moyo mtakatifu na usikate tamaa. Leta chochote usichokielewa mbele Yangu zaidi na hakikisha usiwe na moyo wa mashaka ili uepoke kupata hasara kubwa. Endelea! Endelea! Kaa karibu! Jikwamue kutoka kwa vizuizi na usijichafue. Endelea kwa moyo wote na usirudi nyuma. Lazima utoe moyo wako wakati wote na kamwe usiwahi kuupoteze muda wowote. Roho Mtakatifu daima ana kazi mpya ya kutenda, hutenda mambo mapya na ana nuru mpya kila siku; “kugeuka sura mlimani”—mwili mtakatifu wa kiroho wa Mungu umeonekana! Jua lenye haki hutoa nuru na huangaza, mataifa yote na watu wote wameona uso Wako mtakatifu. Nuru Yangu itaangaza juu ya wale wote wanaokuja mbele Yangu. Maneno yangu ni nuru, yakiwaongoza mbele. Hamtageuka kushoto au kulia mnapotembea lakini mtatembea ndani ya nuru Yangu, na kukimbia kwenu hakutakuwa kazi isiyo na matunda. Lazima muone kazi ya Roho Mtakatifu kwa uwazi na mapenzi Yangu yako pale ndani yake. Siri zote zimefichwa na zitafunuliwa kwenu hatua kwa hatua. Wekeni maneno Yangu akilini wakati wote na mje mbele Yangu kufanya ushirika zaidi na Mimi. Kazi ya Roho Mtakatifu huendelea. Tembeeni katika nyayo Zangu; maajabu makuu yako mbele na yatafunuliwa kwenu moja baada ya lingine. Ni wale tu ambao wanajali, wanaosubiri na ambao wako macho watayaona. Hakikisha usiwe mlegevu. Mpango wa usimamizi wa Mungu unakaribia hatua yake ya mwisho, ujenzi wa kanisa utafanikiwa, idadi ya washindi tayari imewekwa, mwana wa kiume mshindi atafanyika na wataingia katika ufalme na Mimi, kuchukua ufalme Nami, kutawala mataifa kwa fimbo ya chuma na kuwa katika utukufu pamoja!

Sura ya 18

Kujenga kanisa si kitu rahisi cha kufanya! Niliweka moyo Wangu wote katika kulijenga na Shetani angefanya kila kitu ingeweza kuibomoa. Kama unataka kujengwa lazima uwe na maono; lazima uishi maisha kwa Mimi, kuwa shahidi wa Kristo, shikilia Kristo juu kwa juu, na kuwa mwaminifu Kwangu. Hupaswi kutoa visingizio, lakini badala yake kutii bila ya sharti; lazima uvumilie majaribu yoyote, na kukubali yote yanayotoka kwa Mimi. Lazima ufuate chochote Roho Mtakatifu hufanya ili Akuongoze wewe. Lazima uwe na roho hodari na uwezo wa kutofautisha mambo. Ni lazima uelewe watu na usifuate wengine kwa upofu, weka macho yako ya kiroho nga’vu na umiliki elimu kamilifu ya mambo. Watu ambao ni wa akili sawa na Mimi lazima wawe shahidi Kwangu Mimi na kupigana vita vya kuamua dhidi ya Shetani. Lazima uwe umejengwa na kupigana vita. Mimi nipo miongoni mwenu, Ninawasaidia na Mimi ndiye kimbilio lenu.

Shughuli ya kwanza ni kujitakasa, kuwa mtu aliyebadilika, na kuwa na mwenendo imara. Lazima uishi kwa Mimi katika mazingira mazuri na mabaya, na kama uko nyumbani au katika sehemu zingine, usisite kwa sababu ya mtu mwingine, au kwa sababu ya baadhi ya tukio au kitu. Na lazima usimame imara na, kama kawaida, ishi kwa kudhihirisha Kristo na kumdhihirisha Mungu Mwenyewe. Lazima ufanye shughuli zako na kutimiza wajibu wako kama kawaida; hii haiwezi kufanywa mara moja, lakini lazima iendelezwe. Lazima uchukue Moyo Wangu kama moyo wako, dhamira Zangu lazima ziwe mawazo yako, lazima ufikirie hali yote kwa ujumla, ruhusu Kristo Aanzie kwako, na utumikie kwa kushirikiana na wengine. Lazima uende kwa kasi sawa na kazi ya Roho Mtakatifu na ujiegemeze katika mbinu ya wokovu Wake. Lazima ujifanye tupu, na kuwa mtu asiye na hatia na mtu aliye wazi. Lazima ushiriki na kujihusisha kwa kawaida pamoja na ndugu na dada zako, muwe na uwezo wa kufanya mambo katika roho, mpendane, mruhusu nguvu zao zisawazishe udhaifu wako, na kutafuta kujengwa ndani ya kanisa. Ni wakati huo tu ambapo utakuwa na sehemu katika ufalme.

Sura ya 19

Kazi ya Roho Mtakatifu inapoendelea mbele, Mungu kwa mara nyingine tena ametuingiza katika mbinu mpya ya kazi ya Roho Mtakatifu. Matokeo yake, haiepukiki kwamba baadhi ya watu wamenielewa Mimi vibaya na kufanya malalamiko Kwangu. Wengine wamenipinga na kunikataa Mimi, na wamenichunguza Mimi. Hata hivyo, bado Mimi ninasubiri kwa rehema toba yenu na mageuzi. Mabadiliko katika utaratibu wa kazi ya Roho Mtakatifu ni Mungu Mwenyewe kuonekana hadharani. Neno Langu litabaki bila kubadilika! Kwa kuwa ni wewe ninayemwoko, Mimi sitakutelekeza katikati ya safari. Lakini kuna shaka ndani yenu na nyinyi mnataka kurejea mikono mitupu. Baadhi yenu mmeacha kusonga mbele ilhali wengine wanachunguza na kusubiri. Bado wengine wanashughulika na hali hiyo bila kufanya chochote, huku wengine wanafanya tu uigaji. Nyinyi kwa kweli mmeifanya mioyo yenu kuwa migumu! Mmekichukua nilichokisema Mimi kwenu na kukigeuza kuwa majisifu yenu na majivuno. Tafakarini hili zaidi: Haya ni maneno ya huruma na hukumu tu yanayowashukia. Roho Mtakatifu, anapooni kwamba ninyi kwa kweli ni waasi, moja kwa moja anaanza kunena na kuchambua. Lazima muwe na hofu. Msitende mambo kwa kutojali au kufanya lolote kwa pupa. Msiwe bure, wenye kiburi, au kuisitiza kuwa na njia zenu wenyewe! Inawapasa mzingatie zaidi juu ya kuweka neno Langu katika vitendo, na uishi kwa kuyadhihirisha kokote uendako ili yaweze kukubadilisha kwa kweli kutoka ndani na ili uweze kuwa na tabia Yangu. Ni matokeo kama haya tu ndiyo ya kweli.

Kwa minajili ya kanisa kuweza kujengwa, ni lazima uwe wa kimo fulani, na utafute kwa moyo wote na bila kukoma, pamoja na kupokea mchomo na utakaso wa Roho Mtakatifu na kuwa mtu aliyebadilishwa. Ni katika hali kama hiyo ambapo kanisa linaweza kujengwa. Kazi ya

Roho Mtakatifu sasa imewaongozwa nyinyi kuanzisha ujenzi wa kanisa. Kama mkiendelea kutenda mambo kwa njia ilele ya kuchanganyikiwa na uzima kama mlivyofanya zamani, basi hamna matumaini. Lazima mjitayarishe wenyewe na ukweli wote na kuwa na utambuzi wa kiroho, na kutembea njia iliyo kamili kulingana na hekima Yangu. Kwa kanisa kujengwa, ni lazima muwe katika maisha ya roho na siyo tu kuiga kwa juujuu. Maendeleo ya ukuaji katika maisha yenu ni maendeleo sawa na yale ambayo kwayo mmejengwa. Hata hivyo, kumbuka kwamba wale ambao hutegemea vipawa vya kiroho au wale ambao hawawezi kuelewa mambo ya kiroho ama wanakosa hali ya utendaji hawawezi kujengwa, wala wale ambao hawawezi kunikaribia na kuwasiliana na Mimi wakati wote. Wale ambao huyashughulisha mawazo yao na dhana za binadamu au kuishi kwa kufuata mafundisho ya kidini hawawezi kujengwa, na wale ambao huongozwa na hisia zao hawawezi pia. Bila kujali jinsi Mungu anavyokutendea, ni lazima ujiweke chini Yake kabisa. Vinginevyo, huwezi kujengwa. Wale ambao wanajishughulisha na majivuno, kujidai, kiburi, hali ya kuridhika na wanaopenda kuwashushia wengine hadhi na kuringa hawawezi kujengwa. Wale ambao hawawezi kuhudumu kwa uratibu na wengine hawawezi kujengwa. Wale wasio na utambuzi wa kiroho, au kwa upofu hufuata yeyote anayeongoza hawawezi kujengwa, na wale ambao hushindwa kuelewa nia Yangu na ambao huishi katika hali ya zamani hawawezi kujengwa. Wale ambao ni wapole mno kufuata mwanga mpya na hawana maono yoyote kama msingi hawawezi kujengwa.

Kanisa linapaswa kujengwa bila kuchelewa, na Mimi nina hangaiko la kusisitiza kwalo. Unapaswa kuanza kwa kuzingatia uhalisi, na kujiunga na mkondo wa ujenzi kwa kujitoa mwenyewe na nguvu yako yote. Vinginevyo, utakataliwa. Ni lazima ukitelekeze kabisa cha kutelekezwa, na kula na kunywa vizuri kistahilicho kuliwa na kunywewa. Ni lazima uishi kwa kudhihirisha uhalisi wa neno Langu, na hupaswi kuzingatia mambo ya juu juu na yasiyo na mpango. Jiulize, ni kiasi gani umechukua katika neno Langu? Ni kiasi kipi wewe huishi kwa kudhihirisha neno Langu? Ni lazima uwe macho na uache kufanya chochote kwa pupa. Vinginevyo, kitakudhuru tu, siyo kusaidia ukuaji wako mwenyewe katika maisha. Ni lazima uelewe ukweli, ujue jinsi ya kuuweka katika vitendo, na uruhusu neno Langu liwe maisha yako kwa ukweli. Huu ndio ukweli wa jambo!

Kwa kuwa ujenzi wa kanisa sasa umefikia wakati muhimu sana, Shetani anapanga mipango na kufanya juu chini kulibomoa. Hampaswi kuwa wavivu lakini endeleeni kwa uangalifu na mfanye utambuzi katika roho. Bila utambuzi kama huo, mtapatwa na hasara kubwa. Hili si jambo dogo. Ni lazima mlifikirie kama suala la umuhimu. Shetani ana uwezo wa kuonekana kwa uongo na kueneza mifano ambayo hubeba tofauti kubwa ya ubora wa yaliyomo. Watu hutenda mambo kipumbavu na kizembe, na wanakosa utambuzi, ambayo ina maana kwamba nyinyi hamuwezi kuwa macho na shwari wakati wote. Mioyo yenu haipatikani popote. Huduma ni

heshima na kadhalika hasara. Inaweza kusababisha baraka au balaa. Salia mtulivu mbele Yangu na kuishi kwa mujibu wa neno Langu, na kwa hakika utasalia macho na kutumia utambuzi katika roho. Shetani atakapofika, utaweza kujikinga dhidi yake mara moja, na pia kuhisi kuja kwake; utahisi wasiwasi halisi katika roho yako. Kazi ya sasa ya Shetani hujizoeza kwa mabadiliko ya mieleleko. Watu wanapotenda mambo kwa njia ya kuchanganyikiwa na kukosa hadhari, wao hubaki katika utumwa. Lazima usalie macho wakati wote na kuwa waangalifu sana. Usilete ubishi juu ya mafanikio yako mwenyewe na hasara, au kukokotoa kwa ajili ya faida yako mwenyewe. Badala yake, tafuta mapenzi Yangu kufanyika.

Vitu vinaweza kuonekana kufanana lakini ubora wavyo unaweza kutofautiana. Hali kadhalika, nyinyi mnapaswa kutambua watu binafsi na vilevile roho. Lazima ufanye utambuzi na kudumisha kuwa macho kiroho. Sumu ya Shetani inapoonekana, unapaswa kuitambua mara moja; haiwezi kuepuka mwanga wa hukumu ya Mungu. Lazima uwe makini zaidi kwa kusikiliza kwa karibu sauti ya Roho Mtakatifu katika roho yako; usiwafuate wengine bila kufikiri au kukosea kilicho cha uongo kuwa kitu cha kweli. Usimfuate yeyote anayeongoza, ili usije ukapata hasara kubwa. Je, hilo linakufanya ujihisije? Je, mmeona matokeo yake? Hupaswi kwa nasibu kuingilia huduma au kuingiza maoni yako mwenyewe ndani yake, la sivyo Mimi nitakuangamiza. Lakini baya zaidi, kama wewe ukisalia muasi na kuendelea kusema na kufanya unavyotaka, Mimi nitakutenga! Kanisa halihitaji kulazimisha urafiki na watu zaidi; linawataka wale ambao kwa kweli wanampenda Mungu na kweli huishi kulingana na neno Langu. Unapaswa kuwa na ufahamu wa hali yako mwenyewe halisi. Je, si ni kujidanganya wakati maskini hujifikiria kuwa matajiri? Kwa kanisa kujengwa, lazima ufuate roho. Usiendeleo kwa kutenda mambo kwa upofu, lakini kaa katika nafasi yako na kutimiza kazi yako mwenyewe. Hupaswi kupiga hatua nje ya majukumu yako, lakini timiza kazi zozote unazoweza kufanya kwa nguvu zako zote, halafu moyo Wangu utaridhishwa. Si kwamba nyote mtatenda huduma sawa. Badala yake, kila mmoja wenu lazima ufanye wajibu wako mwenyewe na kutoa huduma zenu kwa uratibu na wengine katika kanisa. Huduma zenu hazipaswi kuchepuka kwa upande wowote.

Sura ya 20

Kazi ya Roho Mtakatifu huenda mbele kwa kasi, ikiwaleta nyinyi ndani ya eneo mpya kabisa, ambayo ni kwamba hali halisi ya maisha ya ufalme imejitokeza mbele yenu. Maneno ambayo yamesemwa na Roho Mtakatifu moja kwa moja yamefichua ukina ulio ndani ya moyo wako na kwa hiyo picha moja baada ya nyingine zinaonekana mbele yenu. Wale wote ambao wana njaa na kiu ya haki, ambao wana nia ya kutii kwa hakika watabaki Sayuni na watakaa Yerusalemu Mpya. Kwa hakika wao watapata utukufu na heshima pamoja nami, na kushiriki baraka nzuri pamoja Nami. Sasa kuna baadhi za siri za dunia ya kiroho ambazo bado

hamjaziona, kwa sababu macho zenu za kiroho hazijafunguliwa; vitu vyote bila shaka ni ya ajabu, na miujiza na maajabu, mambo ambayo watu kamwe hawajawahi waza kuyahusu, hatua kwa hatua yatakuja kuwa. Mwenyezi Mungu Ataonyesha miujiza Yake kubwa zaidi ili miisho ya ulimwengu na mataifa yote na watu wote waweze kuiona kwa macho yao yenyewe, na kuona ambako uadhama Wangu, haki na uweza ziko. Ile siku inakuja karibu! Sasa ni muda wa kipeo zaidi—je, mnajitoa au mnastahimili hadi mwisho na kamwe msirudi nyuma? Msiangalie kwa mtu yeyote, jambo au kitu, msiangalie kwa dunia, au waume wenu, watoto au kwa wasiwasi wenu kuhusu maisha, angalieni tu kwa upendo Wangu na rehema, oneni ni nini Nimelipia ili kuwapata nyinyi, ni nini Nilicho, na mambo haya yatatoa tumainisho la kutosha.

Wakati uko karibu sana na mapenzi Yangu lazima yatimizwe kwa haraka yote. Sitatelekeza wale kwa jina Langu lakini Nitawaleta nyote katika utukufu. Lakini inaweza kuonekana kuwa sasa ni muda muhimu. Iwapo mtu hataweza kuchukua hatua hio inayofuata basi wataomboleza kwa wenyewe maisha yao yote na kujuta wakati wamechelewa mno. Sasa vimo vyenu vimewekwa kwa mtihamu wa vitendo, ili kuona kama kanisa linaweza kujengwa na iwapo mwaweza kutii kila mmoja au la. Kukitazamwa kutoka kipengele hiki, kutii kwako kwa kweli ni kutii ambako unachukua na kuchagua—ingawa unaweza kuwa na uwezo wa kutii mtu mmoja, unaweza kuona ni vigumu kumtii mtu mwingine. Kwa kweli hakuna njia ambayo unaweza kuwa mtiifu wakati unategemea dhana za kibinadamu. Hata hivyo mawazo ya Mungu kila mara hupita yale ya mtu! Kristo Alitii hadi kifo na Akafa msalabani. Kristo Hakusema lolote kuhusu hali yoyote au sababu, mradi ilikuwa mapenzi ya Baba Yake, Alitii bila kusita. Utii wako wa sasa ni mdogo mno. Ninawaambia nyinyi nyote, utiifu si kutii watu; badala yake, unamaanisha kutii kazi ya ndani ya Roho Mtakatifu na kumtii Mungu Mwenyewe. Maneno Yangu yanawafanya upya na kuwabadilisha kutoka ndani, vinginevyo nani angemtii nani? Nyinyi nyote ni waasi kwa wengine. Lazima mchukue wakati wa kuifahamu hii, kutii ni nini na jinsi mnaweza kuishi kwa kudhihirisha maisha ya kutii. Lazima mje mbele Yangu zaidi na mshiriki jambo hili, na polepole mtakuja kulielewa, na kwa hiyo kuachilia dhana na uchaguzi ndani yenu. Njia hii ambayo Mimi hufanya mambo ni ngumu kwa watu kuelewa kikamilifu. Sio jinsi watu ni wazuri au wana uwezo—Mimi hutumia wasiojua kabisa, wasio na thamani kabisa ili kufichua uweza wa Mungu na wakati huo Nikipindua dhana, maoni na uchaguzi wa watu wengine. Matendo ya Mungu ni ya ajabu mno, na yanapita makisio ya watu!

Kama kweli unataka kuwa mmoja anayenishuhudia Mimi, lazima upokee ukweli kabisa na si kwa kimakosa. Lazima uzingatie zaidi kwa kuyaweka maneno yangu katika vitendo, kutafuta kwa ajili ya maisha yako kukomaa haraka. Usiende ukitafula mambo ambayo hayana thamani, siyo ya manufaa yoyote kwa uendeleaji wa maisha yenu. Unaweza tu kujengwa wakati maisha yako yamekomaa na ni hapo tu basi unaweza kuletwa katika ufalme—hii inapita shaka lolote.

Bado Ninataka kunena zaidi sana kwako. Nimekupa mengi lakini ni kiasi kipi kweli unakielewa? Ni kiasi kipi cha kile Ninachosema kimekuwa hakika kwa maisha yako? Ni kiasi kipi cha kile Ninasema ambacho unaishi kwa kudhihirisha? Usifanye juhudi zisizoleta manufaa—hutapata lolote hatimaye, na utapata utupu tu. Wengine wamepata faida halisi kwa urahisi sana; Je wewe? Je, unaweza kumshinda Shetani kama huna silaha na hubebi silaha? Lazima uishi zaidi katika utegemezi wa maneno Yangu, na ni silaha bora kabisa kwa ulinzi binafsi. Unapaswa ufahamu: Usikuchukue maneno Yangu kama milki yako; kama huyajui, usiyatafute, usijaribu kuyafahamu au kushiriki nami lakini umeridhika kibinafsi na kujikinai, basi utapata hasara. Unapaswa kutumia somo sasa juu ya kipengele hiki, na ni lazima ujiweke kando na utumie nguvu za wenzio ili kufidia mapungufu yako mwenyewe; usifanye tu lolote unalotaka. Wakati hausubiri mtu yeyote. Maisha za ndugu na madada hukua siku kwa siku, wao hupitia mabadiliko na wote wanafanywa wapya siku kwa siku. Nguvu za ndugu na madada huinuka na hili ni jambo kubwa! Kimbia kwa kasi kwa mstari wa kumalizia, hakuna atakayekuwa na uwezo wa kumshughulikia mtu mwingine, fanya tu juhudi za kibinafsi kushirikiana na Mimi. Wale ambao wana maono, walio na njia mbele, ambao hawajavunjika moyo na ambao kila mara huangalia mbele wanahakikishiwa kuwa watashinda, bila shaka. Sasa ni muda muhimu. Kuwa na uhakika usivunjike moyo au kukataa tamaa. Ni lazima uangalie mbele katika kila kitu na usirudi nyuma, toa kila kitu na uachane na mitego yote na ufuatilie kwa nguvu zako zote. Mradi pumzi moja bado inasalia nawe, vumilia hadi mwisho kabisa; hii tu ndiyo inastahili sifa.

Sura ya 21

Kazi ya Roho Mtakatifu sasa imewaleta katika mbingu mpya na dunia mpya. Kila kitu kinaendelea kufanywa upya, kila kitu ki mikononi Mwangu, kinarudi ulingoni! Kwa dhana zao, watu wanashindwa kulifikiria kwa makini, na kwao haina maana, lakini ni Mimi ambaye niko kazini, na hekima Yangu iko ndani yake. Kwa hiyo mnaweza kukomesha dhana zenu zote na maoni yenu. Mnaweza kujishughulisha na kula na kunywa neno la Mungu katika utii, bila wasiwasi wowote kamwe. Kwa kuwa Nafanya kazi kwa njia hii, Nitachukua jukumu takatifu. Kwa kweli, watu hawana haja ya kuwa namna fulani. Badala yake, ni Mungu anayefanya mambo ya kimiujiza, na kudhihirisha kudura Yake. Watu wasijivune isipokuwa kama wanajivuna kuhusu Mungu. Vinginevyo mtapata hasara. Mungu huwainua masikini kutoka mavumbini, ambako wanyenyekevu wanainuliwa. Mimi nitatumia hekima Yangu katika hali zake zote kulitawala kanisa la watu wote, kutawala mataifa yote na watu wa makabila yote, ili wao wote wawe ndani Yangu, na ili nyote katika kanisa muweze kunitii. Wale ambao hawakutii kabla lazima sasa wawe watiifu mbele Yangu, ni lazima watiiane, wapokeane wao kwa wao, wawe na maisha yanayohusiana, na wapendane, wote wakifaidi kwa weledi wa wenzao katika sehemu ambazo kila mmoja ana udhaifu, wakihudumu kwa uratibu. Kwa njia hii kanisa

litajengwa, na Shetani hatakuwa na nafasi ya kuwatumia watu. Ni hapo tu ambapo mpango Wangu wa usimamizi hautakuwa umeshindwa. Acha Niwape kumbusho jingine hapa. Usiruhusu kutoelewana kuzuke ndani yako kwa sababu mtu fulani ni wa namna fulani, au alitenda mambo kwa njia fulani, likikuacha uwe mtu wa kufifia katika roho. Mimi ninavyoona, hili halifai, na ni kitu bure. Je, Yule unayemwamini si Mungu? Siyo mtu fulani. Shughuli si za aina moja. Kuna mwili mmoja. Kila mmoja hufanya kazi yake, kila mmoja kwa nafasi yake na kufanya kadiri ya uwezo wake—kila cheche ya shauku mwako wa mwanga—kutafuta ukomavu katika maisha. Ni hivyo ndivyo nitakavyoridhika.

Ni lazima mjishughulisha tu na kuwa na amani mbele Yangu. Kuweni katika ushirika wa karibu na Mimi, tafuteni pale ambapo hamuelewi, fanyeni maombi, na muusubiri wakati Wangu. Angalia kila kitu kwa dhahiri kutoka kwa roho. Usifanye mambo bila hadhari, ili kuzuia kupotoka. Ni kwa njia hii tu ambapo kula kwako na kunywa kwa maneno yangu kwa kweli kutazaa matunda. Kula na unywe maneno Yangu mara kwa mara, yatafakari niliyoyasema Mimi, zingatia kutenda maneno Yangu, na uishi kwa kudhihirisha uhalisi wa maneno Yangu; hili ndilo suala muhimu. Maendeleo ya kujenga kanisa ndiyo pia maendeleo ya ukuaji wa maisha. Maisha yako yakiacha kukua, huwezi kujengwa. Kutegemea uasilia tu, kwa mwili, kwa raghba, kwa michango, kwa sifa, bila kujali jinsi ulivyo mzuri, hutajengwa. Lazima uishi katika maneno ya maisha, ishi ndani ya unurishwaji na kuwa katika hali ya kuangazwa kutoka kwa Roho Mtakatifu, jua hali yako halisi, na uwe mtu aliyebadilika. Lazima uwe na ufahamu huo huo ndani ya roho yako, upate nuru mpya, na uwe na uwezo wa kuendelea sawa na mwanga mpya. Lazima uwe na uwezo wa kupata mawasiliano ya karibu na Mimi bila kukoma, uwe na uwezo wa kutegemeza matendo yako katika maisha ya kila siku kwa maneno Yangu, uwe na uwezo wa kuwashughulikia vizuri watu wa kila aina, matukio, na mambo kwa kutegemeza maneno Yangu, shughuli zote katika maisha ukiwa na maneno Yangu kama kiwango chako na ukiishi kwa kudhihirisha tabia Yangu.

Ikiwa unatamani kuelewa na kuyatunza mapenzi Yangu, lazima uyazingatie maneno Yangu. Usifanye mambo kwa pupa. Yale yote ambayo Mimi sikubaliani nayo yataishia vibaya. Baraka huja tu kwa kile ambacho Mimi nimekikubali. Kama Mimi nikisema, litakuwa. Kama Mimi nikiamuru, litasimama imara. Kabisa lazima ninyi msifanye kile ambacho sijaruhusu Mimi, kuepuka kunikasirisha Mimi. Wakati huo hakutakuwa na wakati wa kujuta.

Sura ya 22

Kumwamini Mungu si jambo rahisi kufanya. Ninyi mnajiboronga, mkila kila kitu mkifikiri kuwa haya yote ni ya kuvutia sana, matamu mno! Kuna baadhi ambao bado wanashangilia—wao tu hawana utambuzi katika roho zao. Ni vyema kuchukua muda wa kuuweka katika muhtasari

uzoefu huu. Katika siku za mwisho, kila aina za pepo huibuka kutekeleza majukumu yao, wakikaidi kwa uwazi hatua za mbele za wana wa Mungu na kushiriki katika kuuvunja ujenzi wa kanisa. Mkikuchukulia hii bila kutilia maanani, mkimpa Shetani nafasi za kufanya kazi, italichafua kanisa, watu watakuwa na hofu na kuhisi kukata tamaa, na katika kadhia kubwa, watu kupoteza maono. Kwa njia hii, gharama yenye jitihada ambayo Nimelipa kwa takribani miaka mingi yote inakuwa kazi bure.

Wakati wa ujenzi wa kanisa pia ni wakati wa mhemuko zaidi wa Shetani. Shetani mara kwa mara husababisha usumbufu na kukatiza kupitia kwa watu wachache, na ni wale ambao hawaijui roho au wale waumini wapya ambao wanatekeleza jukumu la Shetani kwa urahisi zaidi. Mara nyingi kwa sababu watu hawaelewi kazi ya Roho Mtakatifu, wananyoosha mikono yao na kufanya mambo kiholela, kulingana kabisa na wanavyopenda wao wenyewe, njia za kufanya mambo na dhana. Shika ulimi wako—hii inasemwa kwa ajili ya ulinzi wako mwenyewe. Sikiliza na utii vyema. Kanisa na jamii ni tofauti. Huwezi tu kusema kile unachopenda, au kusema chochote unachofikiri. Haitawezekana hapa kwa kuwa hii ni nyumba ya Mungu. Mungu hakubali namna watu wanavyofanya mambo. Lazima ufanye mambo kwa kuifuata Roho, ishi kwa kudhihirisha maneno ya Mungu na kisha wengine watakutazama na kupendezwa nawe. Lazima kwanza utatue matatizo yote ndani yako kwa kumtegemea Mungu. Komesha tabia zako potovu na kuwa na uwezo wa kuelewa kweli hali zako mwenyewe na kujua jinsi unapaswa kufanya mambo; endelea kushiriki chochote ambacho hukielewi. Haikubaliki kwa mtu kutojijua. Uponye ugonjwa wako mwenyewe kwanza, na kwa njia ya kula na kunywa maneno Yangu zaidi, kutafakari maneno Yangu, ishi maisha na fanya mambo kwa mujibu wa maneno Yangu; haijalishi ukiwa nyumbani au mahali pengine, unapaswa kumruhusu Mungu atwae nguvu ndani mwako. Uache mwili na uasili. Daima yaruhusu maneno ya Mungu yawe na mamlaka ndani mwako. Hakuna haja ya kuwa na wasiwasi kwamba maisha yako hayabadiliki; utakuja polepole kuhisi kwamba tabia yako imebadilika kiasi kikubwa. Mbeleni, ulikuwa na hamu ya kujionyesha mbele ya watu, hukumtii mtu yeyote au ulikuwa na tamaa ya makuu, mwenye kujidai au mwenye majivuno, na utayatupilia mambo haya mbali hatua kwa hatua. Ukitaka kuyatupilia mbali sasa hivi, basi hiyo haiwezekani! Hii ni kwa sababu binafsi yako ya zamani haitawaruhusu wengine kuigusa, imekita mizizi kabisa ndani yako. Hivyo ni lazima ufanye juhudi za kibinafsi, utii kazi ya Roho Mtakatifu vyema na kikamilifu, utumie hiari yako kushirikiana na Mungu na uwe na nia ya kuyaweka maneno yangu katika vitendo. Ukitenda dhambi, Mungu atakufundisha nidhamu. Unaporejelea na kuwa na ufahamu basi yote yatakuwa mema ndani yako kwa mara moja. Kama unazungumza kwa kujipendekeza, basi utafundishwa nidhamu mara moja kwa ndani. Unaona kwamba Mungu hafurahii jambo la aina hiyo, hivyo ukiliacha mara moja, utakuwa na uzoefu wa amani ya ndani. Kuna baadhi ya waumini wapya ambao hawaelewi hisia

za maisha ni nini au jinsi ya kuishi ndani ya hisia za maisha. Wakati mwingine unashangaa, ingawa hujasema lolote, kwa nini unahisi kutotulia sana kwa ndani? Wakati kama huu ni wazo lako na akili ambavyo vina makosa. Wakati mwingine unayo maamuzi yako mwenyewe, dhana na maoni yako mwenyewe; wakati mwingine unawaona wengine kuwa wadogo zaidi kukuliko; wakati mwingine unafanya hesabu zako mwenyewe za ubinafsi nawe huombi au kujichunguza. Hii ndiyo sababu unahisi kutotulia ndani. Labda unajua tatizo ni nini, kwa hiyo mara moja unaliita jina la Mungu moyoni mwako, unasogea karibu na Mungu nawe utarejeshwa. Wakati moyo wako umevurugika sana na hautulii, lazima kabisa usifikiri kwamba Mungu anakuruhusu kuongea. Hasa wale ambao ni waumini wapya lazima wamtii Mungu vyema katika suala hili. Hisia ambazo Mungu huweka ndani ya mtu ni amani, furaha, uwazi na udhamini. Mara nyingi watu hawaelewi na watatia fujo mambo na kufanya mambo kiholela—haya yote ni makatizo, na kabisa lazima uizingatie. Kama wewe ni wa kuelekea katika hali hii, unapaswa kwanza kuchukua “dawa za kuzuia,” la sivyo utaleta makatizo na Mungu atakupiga. Usiwe mwenye haki wa kibinafsi; zichukue nguvu za wengine na kuzitumia kusawazisha na mapungufu yako mwenyewe, angalia jinsi wengine wanaishi kwa kutegemea maneno ya Mungu na uone kama maisha, vitendo na hotuba zao ni vya thamani ya kujifunza kutoka kwavyo au la. Ukiwaona wengine kuwa chini yako wewe basi ni mwenye haki binafsi, mwenye majivuno ya kibinafsi na huna manufaa kwa yeyote. La muhimu sasa ni kulenga kuhusu maisha, kula na kunywa zaidi maneno Yangu, upate uzoefu wa maneno Yangu, kuyajua maneno yangu, kuyafanya maneno yangu kwa dhati kuwa maisha yako—hili ni jambo kuu. Je, maisha ya mtu ambaye hawezi kuishi kwa kutegemea maneno ya Mungu yanaweza kukomaa? Hapana, hayawezi. Lazima uishi kwa kutegemea maneno Yangu kila wakati. Katika maisha, lazima maneno Yangu yawe kanuni yako ya vitendo. Yatakusababisha kuhisi kuwa kufanya mambo kwa njia fulani ni kile Mungu anafurahia, na kufanya mambo kwa njia nyingine ni kile Mungu anachochukia; polepole, utakuja kutembea katika njia sahihi. Lazima uelewe ni mambo yapi yanatokana na Mungu ni mambo yapi yanatokana na Shetani. Mambo yanayotokana na Mungu hokusababisha kuwa wazi zaidi kuhusu maono, na hokusababisha kusogea karibu na karibu zaidi na Mungu, ukishiriki upendo na ndugu kwa bidii; unakuwa na uwezo wa kutilia maanani mzigo wa Mungu, na moyo wako umpendao Mungu haupungui; kuna njia mbele yako kuitembea. Mambo ambayo hutokana na Shetani hokusababisha kupoteza maono na vyote ulivyokuwa navyo awali vimetoweka; unajitenga na Mungu, huna upendo kwa ndugu nawe una moyo wa chuki. Unakuwa mwenye kukata tamaa, hutaki tena kuishi maisha ya kanisa, na moyo wako umpendao Mungu hauko tena. Hii ni kazi ya Shetani na pia ni matokeo ambayo yameletwa na kazi ya roho mbaya.

Huu sasa ni wakati muhimu. Lazima muendeleo kufanya kazi kwa bidii mpaka dakika ya mwisho kabisa, myaweke wazi macho yenu ya roho ili muweze kutofautisha kati ya mema na

mabaya, na mtumie juhudi nyingi muwezavyo kwa ujenzi wa kanisa. Epukeni vikaragosi wa Shetani, misukosuko ya kidini na kazi ya roho mbaya. Litakaseni kanisa, kufanya mapenzi Yangu itendeke bila kupingwa, na katika wakati huu mfupi sana unaotangulia majanga kweli Nitawafanya kuwa kamili haraka iwezekanavyo, na kuwaleta katika utukufu.

Sura ya 23

Kwa ndugu wote ambao wameisikia sauti Yangu: Mmeisikia sauti ya hukumu Yangu kali na mmevumilia mateso yaliyokithiri. Hata hivyo, mnapaswa kujua kwamba katika sauti Yangu kali kumejificha nia Zangu! Ninawafundisha nidhamu ili muweze kuokolewa. Mnapaswa kujua kwamba kwa wana Wangu wapendwa, Nitawafundisha nidhamu na kuwapogoa na kuwafanya muwe wakamilifu hivi karibuni. Moyo Wangu una hamu sana, lakini ninyi hamuelewi moyo Wangu na hamtendi kulingana na neno Langu. Maneno Yangu leo yanawajia ninyi na kuwafanya kutambua kweli kwamba Mungu ni Mungu mwenye upendo na nyote mmepitia upendo wa dhati wa Mungu. Hata hivyo, pia kuna idadi ndogo ya watu ambao wanajifanya na wanapoon huzuni ya watu wengine pia wao watakuwa na machozi machoni mwao. Kuna wengine ambao—kwa juu—wanaonekana kuwa wadeni wa Mungu na wanaonekana wenye majuto, lakini ndani yao, hawamwelewi Mungu kwa kweli na wala hawana uhakika kumhusu Yeye; badala yake, ni sura ya kinafiki tu. Ninawachukia watu hawa zaidi! Siku moja, watu hawa wataondolewa kutoka katika mji Wangu. Nia Yangu ni kwamba Nataka wale wanaonitaka kwa ari, na wale tu ambao wananifuatilia kwa moyo wa kweli wanaweza kunipendeza—kwani wao Nitawaunga mkono bila shaka kwa mikono Yangu mwenyewe na kuhakikisha kuwa hawatapata majanga yoyote. Watu wanaomtaka Mungu kwa kweli watakuwa tayari kujali mogo wa Mungu na kufanya mapenzi Yangu. Kwa hiyo, ninyi mnapaswa kuingia katika ukweli hivi karibuni na kukubali neno Langu kama maisha yenu—huu ndio mzigo Wangu mkubwa zaidi. Ikiwa makanisa na watakatifu wote wanaingia katika uhalisi na wote waweze kushiriki na Mimi moja kwa moja, wawe uso kwa uso na Mimi, na kutenda ukweli na haki, ni hapo tu ndipo wao ni wana Wangu wapendwa, wale ambao napendezwa nao sana. Watu hawa, Nitawapa baraka zote kubwa.

Sura ya 24

Wakati unakaribia hata zaidi. Amkeni! Watakatifu wote! Nitawatamkia ninyi. Wote wanaosikia wataamka. Mimi ni Mungu ambaye mmekuwa na imani katika kwa miaka hii mingi. Leo nimekuwa mwili na kuja mbele ya macho yenu, na hii inafichua yule ambaye ananitaka kwa kweli, ambaye yuko tayari kulipa gharama yoyote kwa ajili Yangu, ambaye husikiliza neno Langu kwa kweli, na yule ambaye yuko tayari kuuweka ukweli katika matendo. Kwa maana mimi ni mwenyezi Mungu, Ninaweza kuona siri zote za binadamu zilizofichwa gizani, Najua ni nani anayenitaka kwa kweli na Ninajua ni nani anayenipinga Mimi; Ninaweza kuchunguza

mambo haya yote.

Sasa Ningependa kufanya kikundi cha watu ambao wanaupendeza moyo Wangu haraka iwezekanavyo, wale ambao wanaweza kuihurumia mizigo Yangu. Hata hivyo, Siwezi kuacha kusafisha na kutakasa kanisa Langu; kanisa ni moyo Wangu. Ninawadharau watu wote wabaya wanaowazuia msile na kunywa neno Langu. Hii ni kwa sababu kuna watu fulani wachache ambao hawanitaki Mimi kwa kweli. Watu hawa wamejaa udanganyifu, hawaji karibu na Mimi na moyo wao wa kweli, wao ni waovu, na ni watu ambao huzuia utekelezaji wa mapenzi Yangu; wao sio watu ambao huweka ukweli katika matendo. Watu hawa wamejaa kujidai na majivuno, wao ni wenye kutamani makuu vikali, wanapenda kutenda mema kwa nia ya kusimanga, na maneno wanayosema ni mazuri kusikia, lakini kwa siri hawatendi ukweli. Watu hawa waovu wote watakatwa na kuzolewa kabisa; watateseka katika majanga. Maneno haya ni kuwakumbusha na kuwaonya ili msalie kwenye njia inayoupendeza moyo Wangu. Daima rudini katika roho yenu, kwa sababu Ninawapenda wale wanaonipenda kwa moyo wao wote. Kwa kuwa mnanikaribia Mimi, nitawalinda na kuwaweka mbali na wale waovu, Nitawafanya msimame imara nyumbani Kwangu na kuwalinda mpaka mwisho.

Sura ya 25

Mwenyezi Mungu, Baba wa Milele, Mfalme wa Amani, Mungu wetu Anatawala! Mwenyezi Mungu anaweka miguu Yake kwenye Mlima wa Mizeituni. Uzuri ulioje! Sikiliza! Sisi walinzi tunapaza sauti zetu: tunaimba kwa pamoja kwa sauti zetu, kwa kuwa Mungu amerudi Sayuni. Tunaona kwa macho yetu wenyewe ukiwa wa Yerusalemu. Furahieni na kuimba kwa sauti kwa pamoja, kwa kuwa Mungu ametufaraji na Ameukomboza Yerusalemu. Mungu ameweka wazi mkono Wake mtakatifu machoni pa mataifa yote, mtu halisi wa Mungu amejitokeza! Miisho yote ya dunia imeona wokovu wa Mungu wetu.

Ee, Mwenyezi Mungu! Roho saba wametumwa kutoka kwa kiti Chako cha enzi kwa makanisa yote ili kufichua siri Zako zote. Unaketi kwenye kiti Chako cha enzi cha utukufu na Umesimamia ufalme Wako na kuuimarisha na kuushikilia kwa haki; Umeyadhibiti mataifa yote mbele Yako. Ee, Mwenyezi Mungu! Umeilegeza mikanda ya wafalme, Umeyafungua wazi malango ya mji mbele Yako, yasifungike tena. Kwa maana nuru Yako imefika na utukufu Wako unajitokeza na kuangaza uzuri wake. Giza linaifunika dunia na giza totoro imewafunika watu. Ee, Mungu! Hata hivyo, Wewe, umeonekana na kutuangazia mwanga Wako, na utukufu Wako utaonekana kwetu; mataifa yote yatakuja kwa nuru Yako na wafalme kwa upendo Wako. Unayainua macho Yako na kuangalia kila mahali: Wana Wako wanakusanyika mbele Yako, na wanatoka mbali; Mabinti Zako wanabebwa mikononi. Ee, Mwenyezi Mungu! Upendo Wako mkubwa umetushika; ni Wewe unayetuongoza mbele kwenye njia inayouelekea ufalme Wako na

ni maneno Yako matakatifu yanayopenya na kuenea ndani mwetu.

Ee, Mwenyezi Mungu! Tunakushukuru na kukusifu! Hebu tukuheshimu, tukushuhudie, tukusifu, na kukuimbia kwa mioyo safi, yenye utulivu, na thabiti. Hebu tuwe na akili moja na kujengwa pamoja, na Utufanye tuwe wanaoupendeza moyo Wako hivi karibuni, wanaotumika na Wewe. Tunatamani kwamba mapenzi Yako yatekelezwe katika nchi yote bila kuzuiwa.

Sura ya 26

Wanangu, yatilieni maanani maneno Yangu, sikiliza kwa utulivu sauti Yangu na Nitafichua kwako. Uwe na utulivu ndani yangu, kwa maana Mimi ni Mungu wako, Mkombozi wenu wa pekee. Mnatakiwa kutuliza mioyo yenu nyakati zote, mkae ndani yangu; Mimi ni mwamba wako, msaidizi wenu. Msiwe na nia nyingine, lakini mnitegemee kwa mioyo yenu yote na Mimi nitaonekana kwenu kwa hakika—Mimi ni Mungu wenu! Ah, wale wenye mashaka! Hakika hawawezi kusimama imara na hawatapata chochote. Lazima mjue sasa ni wakati gani, ni wakati muhimu kiasi gani. Ni jambo muhimu kivi! Msishughulike huku na kule katika mambo yasiyo na manufaa; sogeeni karibu na Mimi haraka, fanyeni ushirika na Mimi, na nitafichua siri zote kwenu.

Lazima usikilize maneno yote ambayo Roho Mtakatifu anafundisha; usimpuuze. Mara nyingi umesikia maneno Yangu na kisha ukayasahau. Ee wasio na fikra! Umepoteza baraka nyingi sana! Lazima usikilize kwa makini sasa na utilie maanani maneno Yangu, ufanye ushirika zaidi na Mimi na kusogea karibu na Mimi zaidi. Nitakufundisha juu ya chochote ambacho haukielewi, nami Nitawaongoza kwenye njia inayoendelea. Usizingatie sana kushirikiana na watu wengine maana kuna watu wengi sasa wanaohubiri maandishi na mafundisho, na wachache ambao wana uhalisi Wangu kwa kweli. Ushirika wao humfanya mtu achanganyikiwe na asiyehisi, bila kujua jinsi ya kuendelea. Hata ukiwasikiliza, unaishia tu kuelewa kidogo zaidi kuhusu maandishi na mafundisho. Lazima muangalie hatua zenu, mlinde mioyo yenu na kuishi mbele Yangu daima, muwasiliane na Mimi, mnikaribie na nitakuwezesha kuona ambayo huyaelewi. Lazima uangalie kile unachosema, uangalie kwa karibu moyo wako nyakati zote na kutembea katika njia Ninayotembelea.

Haitakuwa muda mrefu sasa, bado kuna muda kidogo uliobaki. Fanya haraka kuacha vitu vyote isipokuwa Mimi na uje unifuata! Sitakutendea vibaya. Mara nyingi mmelewa visivyo matendo Yangu, lakini je, unajua ni kwa kiasi gani Ninakupenda? Ah, huelewi moyo Wangu kabisa. Bila kujali jinsi ulivyokuwa na mashaka na Mimi au ni kiasi gani nilikudai hapo zamani, Sitakumbuka. Lakini bado Niliwachagua ili mweze kwenda mbele na kutenda kulingana na mapenzi Yangu.

Sasa ni wakati ambao hauvumilii kukawia. Ikiwa kutoka sasa na kuendelea mnayo nia nyingine basi hukumu yangu itawafikia. Ukiniacha kwa muda kidogo tu basi utakuwa kama mke wa Lutu. Kasi ya kazi ya Roho Mtakatifu sasa inakusanya kasi na wale ambao hawawezi kwenda kasi sawasawa na mwanga mpya wako katika hatari kubwa. Wale ambao hawaangalii wataachwa; mnapaswa kujilinda wenyewe. Unapaswa kujua kwamba vitu vyote vilivyo katika mazingira yanayo wazunguka vipo hapo kwa ruhusa Yangu, Mimi napanga yote. Oneni wazi na muridhishe moyo Wangu katika mazingira Niliyokupa. Msiogope, Mwenyezi Mungu wa majeshi hakika atakuwa pamoja nawe; Yeye anawasaidia na Yeye ni ngao yenu. Leo watu wana dhana nyingi sana na hili linanifanya Niweze kuonyesha mapenzi Yangu kupitia kwa wale ambao wanadharauliwa na wengine; wale ambao wanajisifu na kujidai, wenye kiburi na majivuno, wenye kutaka makuu na kujionyesha bora wataaibishwa. Ilimradi mnaonyesha kuzingatia kweli juu ya mzigo Wangu basi nitawaandaa kila kitu kwa ajili yenu. Nifuateni Mimi tu!

Sura ya 27

Mungu mmoja wa kweli anayetawala juu ya ulimwengu na vitu vyote—Mwenyezi Mungu, Kristo wa siku za mwisho! Huu ndio ushuhuda wa Roho Mtakatifu, ni ushahidi dhahiri! Roho Mtakatifu anafanya kazi kuwa na ushuhuda kila mahali, ili kusiwe na mtu yeyote mwenye shaka yoyote. Mfalme wa ushindi, Mwenyezi Mungu! Yeye ameushinda ulimwengu, Ameishinda dhambi na kufanikisha ukombozi! Anatuokoa, kundi hili la watu ambao wamepotoshwa na Shetani, na Anatukamilisha kufanya mapenzi Yake. Anatawala dunia nzima, Anaichukua tena na kumfukuza Shetani hadi ndani ya shimo lisilo na mwisho. Anauhukumu ulimwengu, na hakuna mtu anayeweza kukwepa kutoka mikononi Mwake. Anatawala kama Mfalme.

Dunia nzima inafurahia! Inamtukuza Mfalme mshindi—Mwenyezi Mungu! Milele na milele! Unastahili heshima na sifa. Mamlaka na utukufu viwe kwa Mfalme mkuu wa ulimwengu!

Muda ni mfupi, fuata nyayo za Mwenyezi Mungu na uendelea mbele. Kuwa mwangalifu kabisa, uwe mwenye kuufikiria mzigo Wake, uwe mwenye mawazo sawa na Yeye na ujitumie kwa ajili ya mpango Wake wa usimamizi. Lazima usihifadhi mali zako, na hakuna muda mwingi. Zitoe! Usiziweke! Zitoe! Usiziweke!

Sura ya 28

Unaona kwamba muda ni mfupi sana na kazi ya Roho Mtakatifu inavurumisha mbele, ikikusababisha kupata baraka kubwa hivi, kumpokea Mfalme wa ulimwengu, Mwenyezi Mungu, ambaye ni Jua ling'aalo, Mfalme wa ufalme—hii yote ni neema na huruma Yangu. Kuna nini kinachoweza kuwepo kinachoweza kukutoa kwa upendo Wangu? Tafakari kwa makini, usijaribu

kuepa, subiri kwa ustahamilivu mbele Yangu kila wakati na usiwe ukizurura nje daima. Moyo wako lazima ukae karibu na moyo Wangu, na bila kujali kile kinachoweza kukufikia usifanye vitu bila kufikiri au kiholela. Lazima utazame mapenzi Yangu, ufanye chochote Ninachokitaka na kudhamiria kuacha kile ambacho Sikitaki. Ni lazima usitende hisia zako, ila badala yake utende haki kama Mimi; haikubaliki kuwa na hisi za moyoni hata kwa mama na baba yako. Ni lazima uache yote yasiyokubaliana na ukweli na lazima ujitolee na kujitumia kwa ajili Yangu kwa moyo safi unaonipenda Mimi. Usikubali udhibiti wa mtu yeyote, jambo au kitu; alimuradi linapatana na mapenzi Yangu basi lifanye kwa mujibu wa maneno Yangu. Usiogope, kwa kuwa mikono Yangu hukusaidia, na kwa hakika Nitakuinga dhidi ya watu wote wabaya. Unapaswa kuulinda moyo wako, kuwa ndani Yangu nyakati zote, kwa kuwa maisha yako yanaishiwa kwa kutegemea maisha Yangu; ukiniacha basi utanyauka mara moja.

Unapaswa kujua kwamba ni siku za mwisho sasa. Shetani ibilisi, kama simba ambaye ananguruma, anatembea huku na kule, akitafuta watu wa kuwameza. Kila aina ya mapigo yanatokea sasa na kuna aina nyingi tofauti za roho wabaya. Mimi pekee ndiye Mungu wa kweli; Mimi pekee ndiye kimbilio lako. Unaweza tu kujificha sasa katika mahali Pangu pa siri, ndani Yangu tu, na maafa hayatakufika na hakuna janga litakalokuja karibu na hema lako. Ni lazima unikaribie zaidi, ushiriki na Mimi katika mahali pa siri; usishiriki kiholela na watu wengine. Ni lazima uelewe maana katika maneno Yangu—Sisemi kwamba huruhusiwi kushiriki, ni kwamba tu bado sasa huna utambuzi. Katika kipindi hiki, kazi inayofanywa na roho wabaya inaenea kwa haraka. Wanakupa ushirika kupitia kila aina ya watu. Maneno yao yanasikika kuwa mazuri sana, lakini kuna sumu ndani yayo. Ni risasi za kuvutia na kabla ujue yataweka sumu yayo ndani yako. Unapaswa kujua kwamba watu wengi leo si thabiti, kana kwamba wamelewa. Unapokuwa na ugumu na ushiriki na wengine, wanachokuambia ni amri na mafundisho tu, na si kizuri kama kushiriki moja kwa moja na Mimi. Kuja mbele Yangu na umwage kabisa mambo mazee yaliyo ndani yako, fungua moyo wako Kwangu na moyo Wangu hakika utafichuliwa kwako. Moyo wako lazima uwe mwangalifu mbele Yangu. Usiwe mzembe, ila badala yake lazima unikaribie mara kwa mara; hii ni njia ya haraka kabisa ya maisha yako kukua. Ni lazima uishi ndani Yangu na Nitaishi ndani yako na pia Nitatawala kama Mfalme ndani yako, Nikikuongoza katika vitu vyote, na utakuwa na mgao wa ufalme.

Usijidunishe kwa sababu wewe ni mdogo; unapaswa kujitoa Kwangu. Sioni watu wako vipi juu juu au ni wa umri upi. Naona tu iwapo wananipenda kwa kweli au la, na iwapo wanafuata njia Yangu na kutenda ukweli wakipuuza mambo mengine yote. Usijali kuhusu jinsi kesho itakuwa au jinsi siku za baadaye zitakuwa. Alimradi unitegemee kuishi kila siku, basi hakika Nitakuongoza. Usikae kwa fikira kwamba “Maisha yangu ni machanga sana, sielewi chochote,” ambayo ni fikira iliyotumwa na Shetani. Tumia tu moyo wako kunikaribia daima na ufuate

nyayo Zangu hadi mwisho wa njia. Unapoyasikia maneno Yangu ya lawama na onyo na kuzinduka, lazima ukimbie mbele mara moja; usiache kunikaribia, kuwa kasi sawa na nyayo za wanakondoo na endelea kuangalia mbele. Mbele Yangu, ni lazima umpende Mungu wako kwa moyo na nafsi yako yote. Jaribu kuyaelewa maneno yangu zaidi katika njia ya kuhudumu. Katika kutenda ukweli lazima usiwe mwenye moyo dhaifu, ila uwe na moyo wenye nguvu, uwe na azimio na ujasiri wa mtoto wa kiume, na kuwa na moyo mgumu. Ikiwa unataka kunipenda, basi lazima uniridhishe na mambo yote Ninayotaka kutimiza ndani yako. Ikiwa unataka kunifuata, basi lazima utelekeze vyote ulivyo navyo, vyote uvipendavyo, utii kwa unyenyekevu mbele Yangu, kuwa na akili ya kawaida na usijishughulishe kutafiti au kufikiria vitu bila mpango maalum; lazima uwe kasi sawa na kazi ya Roho Mtakatifu daima.

Hapa Nakupa ushauri: Ni lazima ushikilie kwa uthabiti na kutenda yote ambayo Nimetia nuru ndani yako!

Sura ya 29

Je, unajua kwamba wakati unawadia? Hivyo kwa muda mfupi wa hivi karibuni utanitegemea Mimi na kuyatupilia mbali mambo yote kutoka kwako ambayo hayalingani na tabia Yangu: upumbavu, upole wa kuonyesha hisia, mawazo yasiyo wazi, moyo wa upole, nia hafifu, upuuzi, hisia zilizotiwa madoido mengi, kuchanganyikiwa na ukosefu wa utambuzi. Haya lazima yatupiliwe mbali upesi iwezekanavyo. Mimi ndimi mwenyezi Mungu! Mradi tu uko radhi kushirikiana na Mimi, Nitayatibu yote yanayokuuguza. Mimi ni Mungu anayeangalia ndani kabisa ya mioyo ya watu, Naujua magonjwa yako yote na kule ambako dosari zako ziko. Haya ndiyo mambo ambayo yanakuzuia wewe kuwa na maendeleo maishani, na ni lazima yatupiliwe mbali hivi karibuni. La sivyo, mapenzi Yangu hayawezi kutekelezwa juu yako. Kile ambacho mwanga Wangu unamulika juu yake, lazima unitegemea Mimi kukitupilia mbali, Nitegemee kila mara, kuwa karibu na Mimi, na matendo yako lazima yafichue sura Yangu. Shiriki na Mimi zaidi kuhusu kile usichoelewa, na Nitakuongoza, ili kwamba uweze kwenda mbele. Kama huna uhakika, usifanye vitendo vya kiholela; ngoja tu wakati Wangu. Dumisha silika thabiti, usiruhusu hisia zako kali ziwe moto au baridi; lazima uwe na moyo ambao daima inanicha. Kile unachofanya mbele Yangu au nyuma Yangu lazima daima kiwe kulingana na mapenzi Yangu. Usiwe mwenye huruma kwa yeyote kwa niaba Yangu, awe ni mumeo au mmoja wa jamii yako; halikubaliki, haijalishi wao ni wazuri kiasi gani. Lazima uchukue hatua kwa msingi wa ukweli. Ukinipenda Mimi, Nitakuridhia baraka kubwa. Sitamstahimili yeyote anayepinga. Wapende wale Ninaowapenda, na uwachukie Ninaowachukia. Usitilie maanani mtu yeyote, kitu chochote au chombo chochote. Angalia na moyo wako na uone kwa udhahiri watu wanaotumiwa na Mimi, kuwa katika mawasiliano zaidi na wanadamu wa kiroho. Usiwe mpumbavu; lazima utofautishe.

Ngano itakuwa ngano daima na vigugu mwitu havitawahi kua viwe ngano, na ni lazima utambue aina tofauti za watu. Lazima uwe hasa mwangalifu katika usemi wako na uweke miguu yako katika njia ambayo inaupendeza moyo Wangu. Maneno haya lazima yatafakariwe kwa uangalifu. Lazima utupilie mbali uasi wako na ujifanye anayefaa kwa matumizi Yangu upesi iwezekanavyo, ili kwamba moyo Wangu uridhishwe.

Sura ya 30

Amkeni, ndugu! Amkeni, kina dada! Siku Yangu haitakawishwa; wakati ni uhai, na kuushika wakati ni kuokoa uhai! Wakati hauko mbali sana! Mkifanya mitihani ya kuingia katika chuo kikuu na msipite, mnaweza kujaribu tena na mubukue kwa ajili ya mtihani. Hata hivyo, siku Yangu haitakuwa na ucheleweshaji kama huo. Kumbuka! Kumbuka! Ninakuhimiza kwa maneno haya mazuri. Mwisho wa dunia unafunguka mbele ya macho yenu wenyewe, majanga makubwa yanakaribia upesi; Je, maisha yenu ni muhimu au kulala, kula, kunywa, na kuvaa kwenu ndivyo muhimu? Wakati umekuja wa ninyi kufikiria kwa makini mambo haya. Msiwe wenye shaka tena na msiogope kuwa na uhakika!

Ni wa kusikitisha jinsi gani! Jinsi gani walivyo duni! Jinsi gani walivyopofuka! Jinsi gani wanadamu walivyo wakatili! Kwa kweli mnalipuuza neno Langu—je, Ninazungumza nanyi bure? Bado ninyi ni wazembe sana, kwa nini? Kwa nini hivyo? Je, hamjawahi kufikiria kuhusu hilo kabla? Ninasema mambo haya kwa ajili ya nani? Niamini! Mimi ni Mwokozi wenu! Mimi ni Mwenyezi wako! Kesheni! Kesheni! Muda uliopotea hautakuja tena kamwe, kumbuka hili! Hakuna mahali popote duniani ambapo unaweza kununua dawa ambayo itapoza majuto! Kwa hiyo Nitawaambiaje hili? Je, neno Langu halistahili uzingatifu wenu wa makini na kutafakari kwa kurudia? Ninyi ni wazembe sana kwa maneno Yangu na ni msiowajibikia maisha yenu sana; Ninawezaje kustahimili haya? Ninawezaje?

Kwa nini, katika muda huu wote, maisha yanayofaa ya kanisa hayajaweza kuibuka miongoni mwenu? Ni kwa sababu mnakosa imani, hamko tayari kulipa gharama, hamtaki kujitoa wenyewe, na hamko radhi kujitumia wenyewe mbele Yangu. Amkeni, wanangu! Niamini, wanangu! Wapendwa Wangu, kwa nini hamuwezi kufikiria yaliyo ndani ya moyo Wangu?

Sura ya 31

Ninawapenda wale wote wanaonitaka Mimi kwa dhati. Mkilenga kunipenda, hakika Nitawabariki kwa kiasi kikubwa. Je, mnaelewa nia Zangu? Katika nyumba Yangu, hakuna tofauti kati ya hali ya juu na chini. Kila mtu ni mwanangu, Mimi ni Baba yenu, Mungu wenu. Mimi ni mkuu na wa pekee. Ninadhibiti kila kitu ulimwenguni!

Unapaswa “kunitumikia kwa unyenyekevu na katika mafumbo” katika nyumba Yangu. Maneno haya yanapaswa kuwa kama wito wako. Usiwe jani kwenye mti, bali uwe mzizi wa mti na ukite mizizi kwa kina katika uzima. Ingia katika uzoefu halisi wa maisha, uishi kwa kufuata maneno Yangu, unitafute zaidi katika kila suala, na unikaribie zaidi na uwasiliane na Mimi. Usizingatie mambo yoyote ya nje, na usidhibitiwe na mtu, tukio, au kitu chochote, bali uwasiliane tu na watu wa kiroho juu ya kile Nilicho. Elewa nia Zangu, acha uhai Wangu upite miongoni mwenu, na uishi kwa kudhihirisha maneno Yangu na mtii mahitaji Yangu.

Tumia nguvu zako zote katika mambo ambayo Nimekuteua; tumia uwezo wako wote kuuridhisha moyo Wangu. Mimi ni nguvu yako na Mimi ni furaha yako ... Mimi ni kila kitu chako. Nifuatilie tu Mimi. Najua tamaa za kweli za moyo wako na kwamba unajitumia mwenyewe kwa dhati kwa ajili Yangu, lakini unapaswa kujua jinsi ya kujitoa mwenyewe Kwangu nyumbani Mwangu na jinsi ya kunifuata hadi mwisho.

Kanisa ni moyo Wangu na Ninawashwa na hamu kwa ajili ya ujenzi wa kanisa Langu. Unapaswa kujitumia mwenyewe kwa ajili Yangu kwa kujitoa mwenyewe bila kusita hata kidogo, na kuonyesha huruma kwa nia Zangu ili moyo Wangu uridhike.

Sura ya 32

Mwanga ni nini? Katika siku za nyuma kwa kweli mliuona mbadiliko wa kazi ya Roho Mtakatifu kama mwanga. Kuna mwanga wa kweli wakati wote, unaojumuisha ninyi kupata kile Mungu alichokupitia kwa kunikaribia na kushirikiana na Mimi; kuwa na utambuzi katika maneno ya Mungu na kufahamu mapenzi ya Mungu katika maneno Yake—yaani, mnapokula na kunywa, mnahisi Roho wa maneno ya Mungu na kupokea maneno ya Mungu ndani yenu; mkielewa kile Alichokupitia uzoefu na kupokea mwangaza wa Mungu huku mkizungumza na Yeye; na pia kupewa nuru na kuwa na utambuzi mpya katika maneno ya Mungu wakati wote huku mkifikiria na kutafakari. Ukielewa neno la Mungu na uhisi mwanga mpya, basi hutakuwa na nguvu katika huduma yako? Ninyi hujitia wasiwasi sana katika huduma yenu! Hiyo ni kwa sababu ninyi hamjagusa ukweli, hamna uzoefu wa kweli au utambuzi. Kama ungekuwa na utambuzi wa kweli, basi si ungejua jinsi ya kuhudumu? Wakati masuala mengine yanakujia, lazima uyapitie kwa bidii. Ikiwa, katika mazingira rahisi na yenye starehe, unaweza pia kuishi katika mwanga wa uso wa Mungu, basi utauona uso wa Mungu kila siku. Ungeuona uso wa Mungu na uwasiliane na Mungu, je, hungekuwa na mwanga? Ninyi hamuingii katika hali halisi, na daima mko upande wa nje mkitafuta; kutokana na hili hampati chochote na maendeleo yenu katika maisha yanacheleweshwa.

Hapana, msizingatie upande wa nje; badala yake, songeni tu karibu na Mungu kwa ndani,

muwasiliane kwa undani vya kutosha na mfahamu mapenzi ya Mungu; si hivyo mtakuwa na njia katika huduma yenu? Mnapaswa kuwa makini kwa bidii na kutii. Mkifanya tu mambo yote kulingana na maneno Yangu na kuingia katika njia ambazo Ninaonyesha, basi hamtakuwa na njia? Ukipata njia ya kuingia katika uhalisi, basi pia una njia ya kumtumikia Mungu. Ni rahisi! Njoo katika uwepo wa Mungu zaidi, tafakarini maneno ya Mungu zaidi, na utapata kile ambacho umepungukiwa nacho. Utakuwa pia na utambuzi mpya, nuru mpya, na utakuwa na mwanga.

Sura ya 33

Ufalme Wangu unawahitaji wale ambao ni waaminifu, wasio wanafiki, na wasio wadanganyifu. Je, si watu wenye moyo safi na waaminifu duniani hawapendwi na watu? Mimi ni kinyume kabisa cha jinsi ilivyo. Inakubalika kwa watu waaminifu kuja Kwangu; Nafurahia mtu wa aina hii, pia Ninamhitaji mtu wa aina hii. Hii ni haki Yangu hasa. Watu wengine ni wajinga; hawawezi kuhisi kazi ya Roho Mtakatifu na hawawezi kuyaelewa mapenzi Yangu. Hawawezi kuona vyema mazingira ambamo familia yao imo na mazingira yamo, na wanafanya vitu bila kufikiri na kupoteza fursa nyingi za kupata neema. Mara kwa mara, wanajuta matendo yao na wanapokabiliwa na jambo, tena hawawezi kuliona kwa uwazi. Wakati mwingine wanaweza kumtegemea Mungu kupata ushindi, lakini wanapokabiliwa na jambo la aina hiyo tena baadaye, ugonjwa ule wa kitambo unarudi, na hawawezi kuyaelewa mapenzi Yangu. Lakini Siangalii mambo haya, na Sikumbuki dhambi zenu. Badala yake, Nataka kuwaokoa kutoka kwa nchi hii ya fujofujo na kuwaruhusu kuyafanya maisha yenu yawe mapya. Nimewasamehe mara kwa mara. Hata hivyo, sasa ni hatua muhimu zaidi. Hamwezi kuchanganyikiwa tena na hamwezi kusonga mbele namna hiyo tena—kusonga na kusimama. Mtaweza kufikia hatima lini? Ni lazima mfanye kadiri mwezavyo kukimbia kuelekea mwisho bila kusimama. Msizembe katika wakati muhimu zaidi, songeni mbele kwa ujasiri, na karamu karimu iko mbele yenu. Vaeni nguo zenu za harusi haraka na majoho ya haki na mhudhurie chajio cha harusi cha Kristo; furahieni raha ya kifamilia milele na milele! Hamtakuwa wenye huzuni, majonzi na kutanafusi tena kama awali. Kila kitu cha wakati huo kitakuwa kimetoweka kama moshi na uhai uhai uliofufuka wa Kristo tu ndio utakuwa na nguvu ndani yako. Ndani mwako, kutakuwa na hekalu lililotakaswa kwa kusafishwa na kuoshwa, na uhai wa ufufuko ambao umepata utakuwa ndani yako milele hata milele!

Sura ya 34

Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu zote, mwenye kutimiliza yote na Mungu wa kweli mkamilifu! Habebi tu nyota saba, ana Roho saba, ana macho saba, anafungua mihuri saba na kufungua hati ya kukunja yenye maandishi, lakini zaidi ya hayo Yeye anaendesha mapigo saba na vitasa saba na kufungua radi saba; zamani za kale Yeye alipiga vinumbi saba! Vitu vyote

vilivyoumbwa na kufanywa kuwa kamili na Yeye vinapaswa kumsifu, kumpa adhama na kutukuza kiti Chake cha enzi. Ee, Mwenyezi Mungu! Wewe ni kila kitu, Wewe umetimiza kila kitu, na kila kitu kinakamilika na Wewe, vyote vinang'aa, vyote vimekombolewa, vyote viko huru, vyote viko imara na vyenye nguvu! Hakuna chochote kilichofichwa wala kufungwa, na Wewe mafumbo yote yanafumbuliwa. Aidha, Wewe unahukumu halaiki za adui Zako, unaonyesha uadhama Wako, unaonyesha moto Wako unaoendelea vikali, unaonyesha ghadhabu Yako, na hata zaidi Unaonyesha utukufu Wako ambao haujawahi kuonekana awali, wa milele na usio na mwisho! Watu wote wanapaswa kuamka na wanapaswa kushangilia na kuimba bila kusita, wakihimidi mwenye Uweza, yule wa kweli, anayeishi, mkarimu, adhimu na Mungu wa kweli aliye kutoka milele hadi milele. Kiti Chake cha enzi kinapasa kutukuzwa kila wakati, jina Lake takatifu kusifiwa na kutukuzwa. Haya ni mapenzi Yangu—ya Mungu—ya milele na ni baraka zisizo na mwisho ambazo Yeye hutufichulia na kutukarimia! Je, ni nani kati yetu ambaye hairithi? Ili kurithi baraka za Mungu, mtu lazima alitukuze jina takatifu la Mungu na kuja kumwabudu kwa kuzunguka kiti Chake cha enzi. Wale wote ambao wanaenda mbele Yake wakiwa na nia nyingine na dhamira nyingine wanayeyushwa na moto Wake wenye ghadhabu. Leo ni siku ambayo adui Zake watahukumiwa, na pia wataangamia katika siku hii. Hata zaidi ni siku ambayo Mimi, Mwenyezi Mungu, nitafunuliwa na Nitapokea utukufu na heshima. Enyi, watu wote! Inukeni haraka ili mhimidi na kumkaribisha Mwenyezi Mungu ambaye milele na milele hutupa wema wenye upendo, wokovu, na kutupa baraka, huwafanya wana Wake kuwa wakamilifu na kufikia ufalme Wake kwa mafanikio! Hili ni tendo la ajabu la Mungu! Haya ni majaaliwa na mipango ya milele ya Mungu, kwamba Yeye Mwenyewe aje kutuokoa, kutufanya tuwe wakamilifu na kutuleta kwenye utukufu.

Wale wote ambao hawainuki na kuwa na ushuhuda ni wahenga wa vipofu, wafalme wa wasiojua na watakuwa daima wasiojua, wajinga wa milele na vipofu waliokufa daima. Kwa hivyo nafsi zetu zinapasa kuamka! Watu wote wanapaswa kuinuka! Mshangilie, msifu na kumhimidi Mfalme wa utukufu, Baba wa huruma, Mwana wa ukombozi bila kikomo, Roho saba zenye ukarimu, na Mwenyezi Mungu anayeleta moto adhimu wenye ghadhabu na hukumu yenye haki, anayejitosheleza, mkarimu, mwenye Uweza, na mkamilifu. Kiti Chake cha enzi kitatukuzwa milele! Watu wote wanafaa kuona kwamba hii ni hekima ya Mungu, ni njia Yake ya shani ya wokovu, na utimilifu wa mapenzi Yake yenye utukufu. Tusipoinuka na kuwa na ushuhuda, wakati muda utakapokwisha basi hakutakuwa na kurudi nyuma. Iwapo tunapokea baraka au balaa inaamuliwa katika hatua hii iliopo ya safari yetu, kulingana na tunayotenda, kufikiria au kuishi wakati huu. Basi mnapaswa kutenda yapi? Mshuhudieni na kumtukuza Mungu milele; mtukuzeni Mwenyezi Mungu, Kristo wa siku za mwisho—Mungu wa kweli, wa kipekee, na wa milele!

Kuanzia sasa kuendelea unapaswa kuona wazi kuwa wale wote wasiokuwa na ushuhuda kwa Mungu, wasiokuwa na ushuhuda kwa wale wa kipekee, waaminifu kwa Mungu, wale walio na tashwishi kumhusu, wote ni wagonjwa, wafu na wenye kumuasi Mungu! Maneno ya Mungu yamehakikishwa kutoka nyakati za kale: Wale wote ambao hawakusanyiki na Mimi wanatawanyika, na wale wasio upande Wangu wako dhidi Yangu; huu ni ukweli usioweza kubadilishwa uliochongwa jiwani! Wale wasiokuwa na ushuhuda kwa Mungu ni vikaragosi wa Shetani. Watu hawa huja kuwasumbua na kuwadanganya watoto wa Mungu, kukatiza usimamizi wa Mungu, na sharti wawekwe kwenye upanga! Yeyote anayewaonyesha nia nzuri anatafuta maangamizi yake mwenyewe. Unapaswa kusikiza na kuamini tamko la Roho wa Mungu, kutembea kwenye njia ya Roho wa Mungu na kuishi kwa maneno ya Roho wa Mungu, na hata zaidi kusifu kiti cha enzi cha Mwenyezi Mungu milele!

Mwenyezi Mungu ni Mungu wa Roho saba! Yule wa macho saba na nyota saba ndiye Yeye pia; Yeye hufungua mihuri saba, na hati nzima ya kukunja imekunjuliwa na Yeye! Amepiga baragumu saba, na vitasa saba na mapigo saba yako mikononi Mwake, yatakayofunguliwa kwa mapenzi Yake. Ee, ngurumo saba ambazo daima zimefungwa! Wakati wa kuzifungua umewadia! Yule atakayezifungua ngurumo saba tayari ameshaonekana mbele ya macho yetu!

Mwenyezi Mungu! Kila kitu kimekombolewa na kuwa huru na Wewe, hapana ugumu, na kila kitu kinakwenda vizuri! Hakuna kinachothubutu kukupinga au kukuzuia Wewe, vyote hukutii. Chochote kisichotii hufa!

Mwenyezi Mungu, Mungu mwenye macho saba! Vyote viko wazi vikamilifu, vyote ni ng'avu na wazi, vyote vimefunuliwa na kuwekwa wazi. Vyote ni dhahiri kabisa na Yeye, na si tu kuwa Mungu Mwenyewe yuko hivi, lakini pia wana Wake wako hivi vilevile. Hapana yeyote, hakuna kitu chochote, na hakuna hoja yoyote inayoweza kufichwa mbele Yake na wana Wake!

Nyota saba za Mwenyezi Mungu ni ng'avu bashashi! Kanisa limefanywa kuwa kamili na Yeye, Yeye huweka imara mitume wa kanisa Lake na kanisa lote liko ndani ya utoaji Wake. Yeye anafungua mihuri yote saba, na Yeye Mwenyewe analeta mpango wa usimamizi Wake na mapenzi Yake hadi tamati. Hati ndiyo kunga ya lugha ya kiroho ya usimamizi Wake na Amekifungua na kukifunua!

Watu wote wanapaswa kusikiliza baragumu Zake saba zinazopigwa kwa sauti. Kwake, vyote vinajulishwa, kamwe visifichike tena, na hakuna huzuni tena. Vyote vinafunuliwa, na vyote vinashinda!

Baragumu saba za Mwenyezi Mungu ziko wazi, baragumu adhimu na zenye ushindi! Pia ni baragumu zinazowahukumu adui Zake! Katikati ya ushindi Wake, baragumu Yake inatukuzwa!

Yeye hutawala ulimwengu mzima!

Yeye amevitayarisha vitasa saba vya mapigo na vyote vinafunguliwa kwa nguvu kabisa kwa adui Zake kwa kiwango cha juu, na watateketea kwa miale ya moto Wake wenye ghadhabu. Mwenyezi Mungu huonyesha uwezo wa mamlaka Yake na adui Zake wote wanaangamia. Ngurumo saba za mwisho hazitafichwa tena mbele ya Mwenyezi Mungu, zote ziko wazi! Zote ziko wazi! Yeye huwaua adui Zake kwa ngurumo saba, Akiimarisha dunia, Akiifanya imtolee huduma, kamwe kutokuwa isiyofaa!

Mwenyezi Mungu mwenye haki! Tunakutukuza milele! Unastahili sifa zisizoisha, kuhimidiwa kusikoisha na kutukuzwa! Ngurumo Zako saba si tu za hukumu Yako, bali zaidi ni kwa ajili ya utukufu na mamlaka Yako, ili kukamilisha vitu vyote!

Watu wote wanasherehekea mbele ya kiti cha enzi, wakimtukuza na kumsifu Mwenyezi Mungu, Kristo wa siku za mwisho! Sauti zao zinautikisa ulimwengu mzima kama radi! Bila shaka vitu vyote vinakuwepo kwa ajili Yake, na kuinuka kwa ajili Yake. Je, ni nani anayethubutu kutoona utukufu, heshima, mamlaka, hekima, utakatifu, ushindi na ufunuo kuwa sio Zake? Huu ndio utimizaji wa mapenzi Yake na ndio ukamilishaji wa mwisho wa ujenzi wa usimamizi Wake!

Sura ya 35

Ngurumo saba zinatoka katika kiti cha enzi, zinautikisa ulimwengu, zinazipindua mbingu na dunia, na zinaenea kote angani! Sauti hiyo inapenya sana kiasi kwamba watu hawawezi kuepuka wala kujificha kutoka kwayo. Nuru za umeme na ngurumo zinatolewa, mbingu na nchi zinabadilishwa mara moja, na watu wako karibu kufa. Kisha, dhoruba kali sana ya mvua inaufagilia mbali ulimwengu wote kwa haraka sana, ikinyesha kutoka angani! Katika pembe za mwisho kabisa za dunia, kama mvua inayopita katika kila pembe, hakuna waa hata moja linalobaki, na inapofagia vitu vyote toka utosini hadi kidoleni, hakuna kitu kinachofichwa kutoka kwayo wala hakuna mtu yeyote anayeweza kuiepuka. Kama kiasi kidogo chenye baridi cha nuru za umeme, ngurumo zinawafanya watu kutetemeka kwa hofu! Upanga mkali wa kukata kuwili unawaangamiza wana wa uasi, naye adui anakabiliwa na janga, pasipo na popote pa kujificha; wanachanganyikiwa wanapokumbwa na upepo na mvua mkali, na huku wakishtushwa na pigo, wanakufa mara moja ndani ya maji yanayotiririka na kufagiliwa na maji. Wanakufa tu bila namna yoyote ya kuyaokoa maisha yao. Ngurumo saba zinatoka Kwangu nazo zinawasilisha nia Yangu, ambayo ni kuwaangamiza wana wakubwa wa Misri, kuwaadhibu waovu na kuyasafisha makanisa Yangu, ili wote wapendane sana, wafikirie na kutenda kwa njia sawa, na wawe na nia moja nami, na ili makanisa yote katika ulimwengu yaweze kujengwa na kuwa kanisa moja. Hili

ni kusudi Langu.

Ngurumo inaposikika, sauti za kuomboleza zinatokea ghafla. Wengine wanaamka kutoka katika usingizi wao, na, wakiwa wameshtuka sana, wao wanachunguza nafsi zao na kukimbia mara moja mbele ya kiti cha enzi. Wanakoma kufanya hila na kudanganya na kufanya uhalifu, nami Sijachelewa sana kuwaamsha watu kama hao. Naangalia kutoka katika kiti cha enzi. Natazama ndani ya mioyo ya watu. Nawaokoa wale ambao wanitamani sana kwa dhati na kwa ari, nami Ninawahurumia. Nitawaokoa milele wale wanaonipenda mioyoni mwao zaidi ya vingine vyote, wale wanaoyaelewa mapenzi Yangu, na ambao wananifuata hadi mwisho. Mkono Wangu utawashikilia salama ili wasiweze kukabiliana na mandhari haya na hawatapatwa na madhara yoyote. Baadhi, wanapouona umeme huu wenye nuru, wana taabu isiyoelezeka mioyoni mwao na wanajuta kupindukia. Wakiendelea kutenda kwa njia hii, watakuwa wamechelewa sana kusaidika. Ee, yote na kila kitu! Yote yatafanyika. Hii pia ni moja ya njia Zangu za wokovu. Nawaokoa wale wanaonipenda na kuwaangamiza waovu. Kwa hiyo ufalme Wangu utakuwa thabiti na imara duniani na mataifa yote na watu wote, wote ulimwenguni na katika miisho ya dunia, wanajua kwamba Mimi ni uadhama, Mimi ni moto wenye ghadhabu, Mimi ni Mungu anayeutafuta moyo wa ndani kabisa wa kila mtu. Kutoka wakati huu na kuendelea, hukumu ya kiti cha enzi cheupe kikuu imefunuliwa waziwazi kwa raia na imetangazwa kwa watu wote kuwa hukumu imeanza! Bila shaka, wote ambao hawaneni yaliyo mioyoni mwao, wale wanaohisi kuwa na wasiwasi na hawathubutu kuwa na hakika, wale ambao hupoteza wakati, ambao wanayaelewa mapenzi Yangu lakini hawako radhi kuyatenda, sharti wahukumiwe. Lazima mchunguze kwa makini makusudi na nia zenu wenyewe, na mchukue nafasi yenu inayofaa, fanyieni mazoezi kabisa kile Ninachosema, kazieni umuhimu uzoefu wenu wa maisha, msitende kwa shauku kwa nje, lakini yafanyeni maisha yenu yakue, yakomae, yawe imara na yenye uzoefu, na kwa njia hiyo tu ndipo mtaupendeza moyo Wangu.

Wakane vikaragosi wa Shetani na pepo wabaya ambao wanavuruga na kuharibu yale ambayo Ninaunda fursa za kutumia vitu kwa manufaa yao. Lazima wakomeshwe na kuzuiwa kwa ukali na wanaweza tu kushughulikiwa kupitia matumizi ya mapanga makali. Wale walio wabaya zaidi lazima waangamizwe mara moja ili wasiwe tishio katika siku zijazo. Nalo kanisa litakamilishwa, litaondolewa ulemavu wote, nalo litakuwa na afya nzuri, lililojaa uhai na nguvu. Baada ya umeme wenye nuru, radi zinavuma. Hampaswi kupuuza, hampaswi kukata tamaa lakini mfanye kila mwezalo ili mfikie, na hakika mtaweza kuona kile mkono Wangu unachofanya, kile Ninachopata, kile Ninachoacha, kile Ninachokamilisha, kile Ninachoondoa kabisa, kile Ninachoangamiza. Yote haya yatatokea mbele ya macho yenu ili mweze kuona wazi kabisa uweza Wangu.

Kutoka katika kiti cha enzi hadi ulimwengu na miisho ya dunia, ngurumo saba zinasikika. Kikundi kikubwa cha watu kitaokolewa na kutii mbele ya kiti Changu cha enzi. Baada ya huu mwanga wa uzima, watu wanatafuta njia ya kuishi nao hawana budi kuja Kwangu, kupiga magoti katika ibada, midomo yao inaliita jina la Mwenyezi Mungu wa kweli, na kueleza kusihi kwao. Lakini kwa wale wanaonipinga Mimi, watu wanaoishupaza mioyo yao, radi inavuma masikioni mwao na bila shaka sharti waangamie. Haya hasa ni matokeo ya mwisho kwao. Wana Wangu wapendwa ambao ni washindi watakaa Sayuni na watu wote wataona kile watakachokipata, na utukufu mkubwa utatokea mbele yenu. Kwa kweli, hii ni baraka kubwa sana, na ni uzuri ambao ni mgumu kusimulia.

Wakati ambapo sauti za ngurumo saba zinatoka, kuna wokovu wa wale wanaonipenda Mimi, wanaonitamani kwa mioyo ya kweli. Wale wote ambao ni Wangu na ambao Nimewajaalia na kuwachagua wanaweza kuja chini ya jina Langu. Wanaweza kusikia sauti Yangu, ambayo ni wito wa Mungu. Acha wale walio katika miisho ya dunia waone kwamba Mimi ni mwenye haki, Mimi ni mwaminifu, Mimi ni upendo, Mimi ni huruma, Mimi ni uadhama, Mimi ni moto wenye ghadhabu, na hatimaye Mimi ni hukumu isiyo na huruma.

Acha wote ulimwenguni waone kwamba Mimi ni Mungu Mwenyewe halisi na kamili. Watu wote wanaamini kabisa na hakuna mtu anayethubutu kunipinga tena, kunihukumu au kunikashifu tena. Vinginevyo, watakumbana na laana mara moja na msiba utawafika. Watalia na kusaga meno yao tu na watasababisha uharibifu wao wenyewe.

Wacha watu wote wajue, wacha ijulikane katika ulimwengu mzima na katika miisho ya dunia, katika kila nyumba na kwa watu wote: Mwenyezi Mungu ni Mungu mmoja wa kweli. Kila mmoja atapiga magoti ili kumwabudu Yeye na hata watoto ambao wamejifunza tu kuzungumza wataita “Mwenyezi Mungu”! Maofisa hao wenye mamlaka watamwona kwa macho yao wenyewe Mungu wa kweli akiwa mbele yao na pia watasujudu katika ibada, wakiomba huruma na msamaha, lakini kweli wamechelewa sana kusaaidika, kwani muda wao wa kufa umefika. Wanaweza tu kuangamizwa na kuhukumiwa kuelekea kwenye lindi la kina kirefu sana. Nitaikomesha enzi yote, na kuimarisha ufalme Wangu zaidi. Mataifa na watu wote watatii mbele Yangu milele yote!

Sura ya 36

Mwenyezi Mungu wa kweli, Mfalme katika kiti cha enzi, hutawala ulimwengu mzima, Anakabiliana na mataifa yote na watu wote, na kila kitu chini ya mbingu hung'aa kwa utukufu wa Mungu. Viumbe vyote hai katika ulimwengu na hadi miisho ya dunia vitaona. Milima, mito, maziwa, ardhi, bahari, na viumbe vyote viishivyo, katika nuru ya uso wa Mungu wa kweli, na

wamesisimka kana kwamba wameamka kutoka ndotoni, kana kwamba wao ni chipuko zinazochipuka kutoka mchangani!

Ah! Mungu mmoja wa kweli, Huonekana mbele ya dunia. Je, nani anathubutu kumtendea kwa upinzani? Kila mmoja hutetemeka kwa hofu. Hakuna ambao hawajaridhishwa kabisa, mara kwa mara kuomba msamaha, wote kwa magoti yao mbele Yake, vinywa vyote vikimuabudu! Mabara na bahari, milima, mito, vitu vyote kumsifu bila kikomo! Vuguvugu la upepo mwanana wa masika huja na masika kuleta mvua mzuri wa masika. Kama watu wote, mikondo ya mito hutiririka kwa huzuni na furaha, ikitoa machozi ya kuwiwa na kujilaumu. Mito, maziwa, chafuko na mawimbi, yote yanaimba, yakihimidi jina takatifu la Mungu Wa kweli! Sifa hizi zinavuma kwa wazi sana! Mambo yote ya zamani ambayo kwa wakati mmoja yalikuwa yamepotoshwa na Shetani, kila mmoja atafanyia upya, atabadilika, na kuingia katika hali mpya kabisa ...

Hili ni tarumbeta takatifu linasikika! Sikiliza. Sauti hiyo, tamu sana, ni kiti cha enzi kinatoa mlilo, kutangaza kwa mataifa yote na watu, wakati umefika, hatima ya mwisho imefika. Mpango Wangu wa usimamizi umemalizika. Ufalme Wangu huonekana hadharani duniani. Falme za duniani zimekuwa ufalme—wa Mungu—Wangu. Matarumbeta Yangu saba yanasikika kutoka kwenye kiti cha enzi, na ni maajabu gani yatatokea! Watu katika miisho ya dunia watakurupuka pamoja kutoka kila upande kwa nguvu ya lundo na uwezo wa radi, baadhi yao baharini, baadhi yao wakiendesha ndege, baadhi yao watakuja kwa magari ya kila muundo na ukubwa, baadhi yao watakuja mgongoni mwa farasi. Angalia kwa karibu. Sikiliza kwa makini. Hawa wapandao farasi wa kila rangi, pepo kuchochewa, wenye majivuno na waadhimu, kama kuchukua uwanja wa vita, wao hawajali kifo. Katikati ya milio ya farasi na makelele ya watu ya kupiga mayowe wakimwita Mungu wa kweli, wanaume, wanawake na watoto wengi watakanyagwa na kwato zao mara moja. Baadhi yao watakufa, baadhi yao watakuwa wakivuta pumzi yao ya mwisho, baadhi yao watapondwa, pasipo na mtu wa kuwatunza, wakipiga kelele kwa kupagawa, wakilia kwa uchungu. Wana wa uasi! Je, hizi si hatima zenu za mwisho?

Hufurahia kuona watu Wangu, ambao husikia sauti Yangu, na kukusanyika kutoka kila taifa na nchi. Watu wote, uhifadhi Mungu wa kweli daima katika midomo yao, kusifu na kuruka kwa furaha bila kukoma! Wao huushuhudia kwa ulimwengu, na sauti ya ushuhuda wao kwa Mungu wa kweli ni kama sauti ya ngurumo ya maji mengi. Watu wote watasongamana katika ufalme Wangu.

Matarumbeta Yangu saba yatapaza sauti, kuamsha walio lala! Shughulika kwa haraka, muda hujakwisha. Angalia maisha yako! Fungua macho yako na uone ni wakati upi sasa. Ni nini unatafuta? Kuna nini ya kufikiri? Na ni nini kilicho cha kushikilia? Je, inawezekana kuwa bado hujafikiria tofauti katika thamani kati ya kupata maisha Yangu na mambo yote unayopenda na

kushikilia? Acha kuwa makaidi na kucheza kila mahali. Usikose nafasi hii. Wakati huu hautakuja tena! Simama mara moja, tenda kufanyisha roho yako mazoezi, kutumia zana mbalimbali kukuwezesha na kuzuia kila njama na hila za Shetani, na umshinde Shetani, ili kwamba uzeofu wako wa maisha uweze kuwa wa kina zaidi na uweze kuishi kwa kudhihirisha tabia Yangu, ili maisha yako yaweze kukomaa na yawe yenye tajriba na ili uweze daima kufuata nyayo Zangu. Ukiwa bila hofu, ukiwa usiye udhaifu, daima ukisonga mbele, hatua kwa hatua, moja kwa moja hadi mwisho wa njia!

Wakati matarumbeta saba zitatoa sauti tena, itakuwa mwito wa hukumu, hukumu ya wana wa uasi, hukumu ya mataifa yote na watu wote, na kila taifa litajisalimisha mbele ya Mungu. Uso wa utukufu wa Mungu hakika utaonyeshwa mbele ya mataifa yote na watu wote. Kila mtu atakuwa ameridhishwa kabisa, kupiga kelele kwa Mungu wa kweli bila kikomo. Mwenyezi Mungu Atakuwa Mtukufu zaidi, na wanangu watashiriki katika utukufu, kushiriki ufalme nami, kuhukumu mataifa yote na watu wote, kuadhibu maovu, kuokoa na kuwa na huruma juu ya watu ambao ni Wangu, kuleta uthabiti na utulivu kwa ufalme. Kupitia sauti ya matarumbeta saba, kundi kubwa la watu litaokolewa, kurudi mbele Yangu kupiga magoti na kuabudu, kwa sifa daima!

Wakati matarumbeta saba zitatoa sauti mara nyingine tena, hilo litakuwa tukio la hitimisho la mwisho wa enzi, mlipuko wa sauti wa tarumbeta ya ushindi dhidi ya ibilisi Shetani, saluti katika mwanzo wa maisha ya wazi wa ufalme duniani! Sauti hii ya kifahari sana, sauti hii inayonguruma pande zote za kiti cha enzi, mlipuko wa sauti ya tarumbeta inayotikisa mbingu na dunia, ni ishara ya mpango Wangu wa usimamizi, na hukumu ya Shetani, kuadhibu duniani hii ya zamani kwa kifo kabisa, jahanamu! Huu mlipuko wa sauti ya tarumbeta unaashiria kwamba lango la neema ni linafungika, kwamba uhai wa ufalme utanza duniani, ambayo ni kamilifu kabisa. Mungu Huokoa wale wanaompenda. Mara tu watakaporudi kwa ufalme Wake, watu duniani watakabili njaa, ndwele ya kufisha, na mabakuli saba ya Mungu, tauni saba zitaanza kutumika kwa mfululizo. Mbingu na dunia zitapita, lakini neno Langu halitapita!

Sura ya 37

Kwa kweli hamna imani mbele Yangu na mara kwa mara mnajitegemea wenyewe kufanya mambo. “Hamuwezi kufanya chochote bila Mimi!” Lakini nyinyi watu wapotovu daima mnachukua maneno Yangu ndani ya sikio moja na linatokea nje ya lile nyingine. Maisha siku hizi ni maisha ya maneno; bila maneno hakuna maisha, hakuna uzoefu, wala hakuna imani. Imani iko katika maneno; ni kwa kugegemea zaidi ndani ya maneno ya Mungu ndio mnaweza kuwa na kila kitu. Msihangaike kuhusu kutokomaa; maisha huja kupitia kwa ukuaji, sio kupitia kuhangaika.

Daima nyinyi ni wepesi wa kuwa na wasiwasi na hamsikizi maagizo Yangu. Daima mnataka kuzidi mwendo Wangu. Hilo linahusu nini? Ni tamaa ya makuu yasiyostaarabika ya watu. Mnapaswa kutofautisha wazi kile kinachokuja kutoka kwa Mungu na kile kinachotoka kwenu. Shauku haitasifiwa kamwe mbele Yangu. Ninataka muwe na uwezo wa kunifuata kwa dhati hadi mwisho kuanzia mwanzo. Lakini mnaamini kwamba kutenda hili ni kujitolea kwa Mungu. Wanadamu vipofu! Mbona msije mbele Yangu zaidi na kutafuta? Mbona mnatenda tu bila kufikiri? Lazima muone kwa wazi! Bila shaka sio mtu ambaye anafanya kazi sasa, lakini badala yake ni Mkuu wa yote, Mungu mmoja wa kweli—Mwenye uweza! Ni lazima msipuuze, bali daima mshikilie kila kitu mlichio nacho, kwa sababu siku Yangu i karibu. Je, bado hamwamki wakati huu? Je, bado hamuoni wazi? Bado mnaandamana na dunia na hamuwezi kujitenganisha nayo. Kwa nini? Je, kweli mnanipenda? Je, mnaweza kufichua wazi mioyo yenu Kwangu ili Niione? Je, mna uwezo wa kujitoa kikamilifu Kwangu?

Fikiria kuhusu maneno Yangu zaidi, na daima muwe na ufahamu dhahiri kuyahusu. Msiwe wa kuvurugwa na kuchanganyikiwa au kuwa wa shingo upande. Tumia muda zaidi mbele Yangu, pokea maneno Yangu yaliotakaswa zaidi, na msielewe visivyo nia Yangu. Ni nini zaidi Ninaweza kusema kwenu? Mioyo ya watu ni ngumu na fikira za watu ni nzito mno. Daima wao hufikiri kupita tu kunatosha, na wao daima hufanyia utani maisha yao. Watoto wajinga! Sio mapema, sio muda wa kucheza tu. Mnapaswa kuyafungwa macho yenu na kutazama wakati. Jua li karibu kuvuka upeo wa macho na kuangaza dunia. Fungua macho yenu na muangalie kwa uangalifu, msiwe wazembe.

Mnachukua jambo kubwa kama hili kwa wepesi na kulichukulia hivi! Moyo Wangu una wasiwasi, lakini kunao wachache ambao hufikiria kuhusu moyo Wangu na wana uwezo wa kusikia shawishi Zangu nzuri na kusikiliza ushauri Wangu! Huu ujumbe ni mgumu, lakini kunao wachache kati yenu nyinyi ambao wanaweza kushiriki sehemu ya mzigo kwa ajili Yangu, bado mna msimamo huu. Ingawa mmeendelea kiasi ikilinganishwa na hapo zamani, hampaswi kubaki katika hali hii! Nyayo Zangu zinasonga mbele kwa kasi, lakini bado mko kwa aina hii ya mwendo. Mnawezaje kwenda kwa mwendo sawa na nuru ya leo na kwenda kwa mwendo sawa na hatua Zangu? Msisite tena. Nimewasisitizia nyinyi tena na tena, siku Yangu haitacheleweshwa tena!

Nuru ya leo hata hivyo ni ya leo. Haiwezi kulinganishwa na nuru ya jana na haiwezi kulinganishwa na nuru ya kesho. Ufunuo mpya, nuru mpya inazidi nguvu kila siku na inang'aa zaidi kila siku. Jiondoeni kutoka kwa kutunduwa kwenu, msiwe wajinga tena, msiwe wenye kushikilia ukale tena, msicheleweshe wakati Wangu tena wala msipoteze muda Wangu bure.

Tazama! Tazama! Niombeni Mimi zaidi, tumia muda zaidi mbele Yangu, na bila shaka

mtapata kila kitu! Amini kwamba kwa njia hii bila shaka mtapata kila kitu!

Sura ya 38

Si kwamba imani yako ni nzuri au safi, lakini badala yake, kazi Yangu ni ya ajabu! Kila kitu ni kwa sababu ya rehema Zangu! Hupaswi kuwa na tabia potovu ya ubinafsi au kiburi hata kidogo, vinginevyo Sitakufanyia kazi. Lazima uelewe wazi kwamba iwapo watu wanaanguka au kusimama imara si kwa sababu yao; ni kwa sababu Yangu. Leo, kama huelewi vizuri hatua hii, hakika utashindwa kuingia katika ufalme! Lazima uelewe kwamba kile kinachofanywa leo ni kazi ya ajabu ya Mungu; hakina uhusiano na mwanadamu. Je, matendo ya mwanadamu yana umuhimu gani? Wakati si mwenye ubinafsi, wenye kiburi, na mwenye majivuno, anakatiza usimamizi wa Mungu na kuharibu mipango Yake. Eh, ninyi wapotovu! Lazima unitegemee Mimi leo; usipofanya hivyo, leo Nitakuambia kwamba hutafanikisha chochote kamwe! Yote yatakuwa bure na shughuli zako hazaitakuwa na maana!

Usipoteze wakati au kusita; leo kila mmoja anayenipenda atakuwa na kazi Yangu ya ajabu ikifanywa juu yake. Siwahitaji wale ambao hawajinyenyekezi, na leo Ninawatumia tu wale ambao wananyenyekezwa kabisa. Ni wale tu wanaonipenda kwa moyo wa kweli, wanaodharauliwa na wengine, wanaoweza kujifunua kabisa Kwangu, Nitakuwa wazi kwako kabisa. Nitakuwezesha kuelewa nia Zangu na wakati wote upo mbele Yangu ukipokea baraka Zangu. Leo wale wanaojitumia kwa ajili Yangu, kujitolea kwa ajili Yangu, na kubeba mizigo kwa ajili Yangu, kamwe Sitawatendea isivyo haki, na hivyo haki Yangu inafichuliwa. Usilalamike kunihusu Mimi; neema Yangu inakutosha. Ni afadhali uje kuichukua ili uweze kuonja utamu usio na kifani. Hii haitasababisha tu upendo kwa ajili Yangu ndani yako, bali itaimarisha upendo huo vile vile.

Kazi Yangu hutekelezwa hatua kwa hatua, na bila shaka siyo isiyojali, au iliyokanganywa. Ili kunifuata, lazima pia mfanye mambo kwa njia hii. Angalieni mwenendo Wangu na mjifunze kutoka Kwangu; kwa njia hii, mkifuata nyayo Zangu basi mtaletwa katika udhihirisho wa ufalme. Shangilia kwa sauti moja! Wanangu! Kazi ya Mungu itafanikishwa juu yenu kundi la watu. Je, hamhisi kuwa mmebarikiwa?

Kwa kweli ni vigumu kuelewa! Nimewaleta hapa leo ili mweze kuiona kazi Yangu ya ajabu!

Sura ya 39

Fungueni macho yenu na muangalie, na mnaweza kuona nguvu Zangu kuu kila mahali! Mnaweza kuwa na uhakika na Mimi kila mahali. Ulimwengu na anga vinaeneza nguvu Zangu

kuu. Maneno ambayo Nimenena yametimia katika ongezeko la joto la hali ya hewa, katika mabadiliko ya hali ya hewa, katika ukosefu wa ukawaida ndani ya watu, katika ulemavu wa elimumwendo ya kijamii, na katika udanganyifu ulio mioyoni mwa watu. Jua linakuwa jeupe na mwezi unakuwa mwekundu; vyote haviko katika usawa. Je, kweli bado hamuoni mambo haya?

Nguvu kuu ya Mungu inafichuliwa katika haya. Ni bila shaka, Yeye ni Mungu mmoja wa kweli—Mwenyezi—ambaye watu wamemwandama kwa miaka mingi! Nani anayeweza kufanya vitu viwepo kwa kunena maneno tu? Mwenyezi Mungu wetu pekee. Punde Anapozungumza, ukweli huonekana. Unawezaje kukosa kusema kwamba Yeye ni Mungu wa kweli?

Najua moyoni kwamba ninyi nyote mko tayari kushirikiana na Mimi, na Ninaamini kwamba wateule Wangu, ndugu Zangu wapendwa wote wana matarajio ya aina hii, lakini hamwezi kabisa kuingia au kutenda kwa kweli, na hamwezi kusalia watulivu na wanyamavu mnapokuwa mkikabiliwa na tukio la hali halisi. Hamyajali kamwe makusudi ya Mungu, na mnaweka maslahi yenu wenyewe kwanza na kutenda ninyi wenyewe bila kusubiri. Hebu Niwaambie, njia hii haitaridhisha nia Zangu kamwe! Mwana! Nipe tu moyo wako kabisa. Kuwa wazi! Sitaki fedha zako, au mali yako, na wala Sitaki uje mbele Yangu kunitumikia kwa bidii, kwa udanganyifu au kwa akili finyu. Kuwa mtulivu na mwenye moyo safi, subiri na utafute matatizo yanapotokea, nami Nitakupa jibu. Usiwe na shaka! Kwa nini huamini kamwe maneno Yangu kuwa ya kweli? Kwa nini huwezi kuamini katika maneno Yangu? Wewe ni mkaidi kwa kiwango kikubwa mno na hata kwa wakati kama huu wewe bado uko namna hii; wewe ni mjinga sana, na hujapata nuru kabisa hata kidogo! Je, ni kiasi gani cha ukweli muhimu sana ambacho unakumbuka? Je, umeupitia kweli? Unatatanishwa na kutenda kiholela na kwa haraka unapokumbana na matatizo! Jambo kuu leo ni kwamba mwingie katika roho na kufanya ushirika na Mimi zaidi, kwa njia hiyo hiyo mioyo yenu wenyewe hutafakari maswali mara kwa mara. Je, mnaelewa? Hili ni muhimu! Kutenda kulikochelewa kwa kweli ni tatizo. Harakisheni, na msichelewe! Watu wanaosikia maneno Yangu na wasichelewe bali wayatende mara moja watabarikiwa sana! Nitawapa maradufu! Msiwe na wasiwasi! Fanyeni kama Ninavyosema, bila kuchelewa hata sekunde moja! Fikira zenu zenu za kibinadamu mara nyingi huwa hivi, na ninyi mna uelekeo wa kuahirisha mambo, daima mkichelewesha kile kinachopaswa kufanywa leo hadi kesho. Ninyi ni wavivu na wasio waangalifu sana. Maneno hayawezi kuelezea jambo hilo! Mimi Sipigi chuku—huu ni ukweli. Kama huamini hili, basi jichunguze na iangalie kwa makini hali yako mwenyewe, na utagundua kwamba hivi ndivyo ilivyo kweli!

Sura ya 40

Kwa nini ninyi ni bozi sana? Kwa nini hamsikii? Makumbusho kadhaa hayajawazindua; hili linanihuzunisha. Kwa kweli Sipendi kuwaona wanangu namna hii. Moyo Wangu unawezaje

kustahimili hili? Ah! Lazima Niwafundishe kwa mkono Wangu mwenyewe. Mwendo Wangu unaendelea kuwa wa kasi. Wanangu! Inukeni haraka na mshirikiane na Mimi. Nani wanajitumia kwa dhati kwa ajili Yangu sasa? Ni nani anayeweza kujitolea kikamilifu bila malalamiko hata kidogo? Daima ninyi ni wenye kutosikia na wapumbavu! Ni wangapi wanaoweza kuwa wenye huruma kwa hisia Zangu, na ni nani anayeweza kuelewa kwa kweli Roho ya maneno Yangu? Ninaweza tu kusubiri kwa hamu na kuwa na matumaini; nikiona kwamba kila moja ya hatua zenu haiwezi kuuridhisha moyo Wangu, Ninaweza kusema nini? Wanangu! Kila kitu ambacho Baba anafanya leo ni kwa ajili ya wana Wangu. Kwa nini wanangu hawawezi kamwe kuuelewa moyo Wangu, na kwa nini wana Wangu daima wanisababisha Mimi, Baba yenu, kuwa na wasiwasi? Wanangu watakua lini, wasinisababishe kuhangaika, na kunikubalia kuwa mtulivu kuwahusu? Wanangu wataweza kuishi kwa kujitegemea lini, kusimama, na kurahisisha mizigo iliyo mabegani mwa Baba? Ninawalilia wanangu kimya kimya tu, nami Ninaeleza kila kitu kwa ajili ya kukamilisha mpango wa usimamizi wa Mungu na kuwaokoa wana Wangu, wapendwa Wangu. Sina chaguo lingine.

Ahadi Zangu zimetimia na zinadhihirika mbele ya macho yenu. Kwa nini usiufikirie moyo Wangu? Kwa nini? Kwa nini? Hadi sasa, umehesabu: Ni mambo mangapi umeyafanya ambayo yameuridhisha moyo Wangu, na ni mambo mangapi umefanya yaliyolirutubisha na kulilisha kanisa? Tafakari haya kwa makini na usiwe holela. Usiache hata hali moja yenye ukweli. Huwezi tu kulenga umbo la nje na kupuuza kiini. Nyakati zote lazima uchunguze kama kila neno lako na tendo lako na kila hatua yako imepitia hukumu mbele ya kiti cha Kristo, na kama umebadilika na kuwa na sura ya mtu mpya—si kwa kuiga, lakini badala yake kutoka ndani ya maonyesho ya maisha. Usicheleweshe maisha yako ili kuepuka kupitia mateso. Harakisha na urekebishe hali hii, uridhishe moyo Wangu, na uzingatie kanuni za mwenendo: Fanya mambo kwa haki na maadili na uridhishe moyo Wangu. Usiwe holela. Je, utakumbuka hilo?

Sura ya 41

Kuhusu shida zinazoibuka kanisani, usiwe na mashaka mengi. Kanisa linapojengwa haiwezekani kuepuka makosa, lakini usiwe na wasiwasi unapokabiliwa na shida hizo; kuwa mtulivu na makini. Sijawaambia hivyo? Omba Kwangu mara nyingi, na Nitakuonyesha kwa wazi nia Zangu. Kanisa ni moyo Wangu na ni lengo Langu la msingi, Naweza je kutolipenda? Usiogope, mambo kama haya yanapotendeka kanisani, yote yanaruhusiwa na Mimi. Simama na kuzungumza kwa niaba Yangu. Kuwa na imani kwamba mambo na masuala yote yanaruhusiwa na kiti Changu cha enzi na yote yana nia Zangu ndani yayo. Ukiendelea kushiriki kwa hiari kutakuwa na shida, umefikiri kuhusu matokeo? Hii ni aina ya jambo ambalo Shetani atatumia kwa manufaa yake. Kuja mbele Yangu mara nyingi. Nitazungumza kwa uwazi: Kama utafanya

kitu bila kuja mbele Yangu, basi usifikiri unaweza kukikamilisha. Ni ninyi ambao mmeniweka katika nafasi hii.

Usivunjike moyo, usiwe dhaifu, Nitakufichulia. Njia ya kwenda kwa ufalme sio laini hivyo, hakuna kitu kilicho rahisi hivyo! Unataka baraka zije kwa urahisi rahisi, sivyo? Leo kila mtu atakuwa na majaribio machungu ya kukumbana nayo, vinginevyo moyo wa upendo ulio nao Kwangu hautakuwa wenye nguvu zaidi na hutakuwa na upendo wa kweli Kwangu. Hata kama majaribu haya yanajumuisha hali ndogo tu, kila mtu lazima ayapitie; ni kwamba tu ugumu wa majaribu utakuwa tofauti kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Majaribu ni Baraka kutoka Kwangu, na ni wangapi kati yenu ambao huja mbele Yangu na kupiga magoti mkiomba baraka Zangu? Watoto wapumbavu! Wewe daima huhisi kwamba maneno machache ya bahati huhesabika kama baraka Yangu, lakini huhisi kuwa uchungu ni moja ya baraka Zangu. Wale wanaoshiriki katika uchungu Wangu bila shaka watashiriki utamu Wangu. Hiyo ni ahadi Yangu na baraka Zangu kwenu. Usisite kula na kunywa na kufurahia. Wakati giza litapotea hapa kutakuwa na nuru. Huwa kuna giza kuu kabla ya alfajiri; baada ya wakati huu kutakuwa na mwangaza zaidi polepole, na baadaye jua litainuka. Usiogope au kuwa mwepesi kutishwa. Leo Ninawaunga mkono wana Wangu na kushika mamlaka Yangu kwa ajili.

Inapofikia shughuli za kanisa, usikwepe jukumu lako. Ukilileta suala hilo mbele Yangu kwa uangalifu sana, utapata njia. Jambo dogo kama hili linapotokea, unakuwa na woga na wasiwasi, hujui la kufanya? Nimesema mara nyingi, “Nikaribie mara kwa mara!” Je, mmeweka vitu Nilivyowaambia mweke katika vitendo kwa uangalifu sana? Mmetafakari neno Langu mara ngapi? Kwa hivyo, hamna utambuzi wowote ulio wazi. Hicho si kitu mlichosababisha? Mnawalaumu wengine, mbona hamjichukii? Mmepurugua vitu na baadaye bado hamko makini sana na bado mko wazembe; mtazingatia neno Langu.

Watiifu na wanyenyekevu watapata baraka nyingi. Kanisani, mtasimama imara katika ushuhuda wenu Kwangu, mshikilie ukweli—haki ni haki na mabaya ni mabaya—wala msichanganye nyeusi na nyeupe. Mtakuwa vitani na Shetani na lazima mumshinde kabisa ili asiinuke kamwe. Lazima mtoe kila kitu kulinda ushuhuda Wangu. Hili litakuwa lengo la matendo yenu, usisahau jambo hili. Lakini sasa, mmepungukiwa katika imani na uwezo wa kutofautisha vitu na ninyi daima hamuwezi kuelewa neno Langu na nia Zangu. Hata hivyo, usiwe na wasiwasi; kila kitu kinaendelea kulingana na hatua Zangu na wasiwasi huzaa shida tu. Shinda kwa muda zaidi mbele Yangu na usitilie maanani chakula na nguo kwa mwili wa asili. Tafuta nia Zangu mara nyingi, na Nitakuonyesha wazi ni nini. Pole pole utapata nia Zangu katika kila kitu, ili kwamba nitakuwa na njia ya kwenda ndani ya kila mtu bila vizuizi. Itauridhisha moyo Wangu na mtapata baraka pamoja na Mimi milele na milele!

Sura ya 42

Matendo ya Mwenyezi Mungu yalivyo makuu! Ni ajabu iliyoje! Jinsi gani ilivyo ya kushangaza! Tarumbeta saba zinatoa sauti, ngurumo saba zinatotoka, na bakuli saba zinamwangwa—hivi vitadhihirika wazi kuanzia sasa kuendelea, na hakuwezi kuwa na shaka. Upendo wa Mungu hutujia kila siku. Ni Mwenyezi Mungu pekee Anayeweza kutuokoa; kama tunakabiliwa na bahati mbaya au tunapokea baraka yote yamo mikononi Mwake kabisa, na sisi binadamu hatuna njia ya kuamua hili. Wale wanaojitoa wenyewe kwa moyo wao wote hakika watapokea baraka tele tele, ilhali wale wanaotafuta kulinda maisha yao wanapoteza tu maisha yao; vitu vyote na mambo yote yamo mikononi mwa Mwenyezi Mungu. Usisitishe hatua zako tena. Mabadiliko ya kiwango kikubwa yanakuja mbinguni na duniani, ambayo mwanadamu hawezi kujificha kutoka kwayo. Hakutakuwa na chaguo lingine kwake ila kulia kwa uchungu mkubwa. Fuata kazi ambayo Roho Mtakatifu anafanya leo. Unapaswa kuwa dhahiri ndani yako kuhusu hatua ambayo kwayo kazi Yake imeendelea, bila haja ya kukumbushwa na wengine. Rejea sasa katika uwepo wa Mwenyezi Mungu mara nyingi kadiri ya uwezo wako. Mwombe kila kitu. Hakika Atakupa nuru ndani na, katika nyakati muhimu kabisa, Atakulinda. Usiwe na hofu! Tayari Anamiliki nafsi yako yote. Kwa ulinzi Wake na huduma Yake, kuna nini cha wewe kuogopa? Leo mafanikio ya mapenzi ya Mungu umekaribia, na yeyote anayehofu anaelekea tu kupoteza. Kile Ninachokwambia ni ukweli. Fungua macho yako ya kiroho: Mbingu inaweza kubadilika ghafla, lakini kuna nini cha wewe kuhofu? Kwa ishara ndogo kabisa ya mkono Wake, mbingu na dunia vinaangamizwa mara moja. Kwa hivyo mwanadamu anaweza kufaidi nini kwa kuhofu? Je, si vitu vyote viko mikononi mwa Mungu? Akiziamuru mbingu na dunia kubadilika, basi zitabadilika. Akisema tunapaswa kukamilishwa, basi tutakamilishwa. Mwanadamu hapaswi kuwa na haraka, bali anapaswa kuendelea kwa utulivu. Hata hivyo, unapaswa, kadiri ya uwezo wako, uwe msikivu sana na uwe macho. Mbingu inaweza kubadilika ghafla! Hata mwanadamu ayafungue macho yake wazi vipi, hataweza kuona kitu chochote. Kuwa mwangalifu sasa. Mapenzi ya Mungu yametimizwa, mradi Wake umekamilika, mpango Wake umefanikiwa, na wanawe wote wamefika kwenye kiti Chake cha enzi. Kwa pamoja wote wanakuja kukaa ili kuyahukumu mataifa yote na watu wote pamoja na Mwenyezi Mungu. Wale ambao wamekuwa wakilitesa kanisa na kuwadhuru wana wa Mungu watakutana na adhabu kali: Hilo ni bila shaka! Wale ambao hujitoa kwa dhati kwa Mungu, wanashikilia kila kitu, bila shaka Mungu atawapenda milele na milele, bila kubadilika kamwe!

Sura ya 43

Je, Sijawakumbusha? Msiwe wenye hofu; ninyi hamjanisikiliza tu, watu wasio na fikira ninyi! Je, mtaweza kuuelewa moyo Wangu lini? Kila siku kuna nuru mpya, kila siku kuna

mwanga mpya. Ni mara ngapi mmeuelewa kwa ajili yenu wenyewe? Je, Sijawaambia Mwenyewe? Bado ninyi ni wa kukaa tu kama wadudu ambao watasonga tu wanaposukumwa, lakini hamwezi kuchukua hatua ya kushirikiana na Mimi, kuufikiria mzigo Wangu. Ningependa kuona tabasamu zenu changamfu na za kupendeza, kuona mwenendo wa Wanangu ulio wa vitendo na mchangamfu, lakini Siwezi. Badala yake, ninyi mmepungukiwa na akili, ni wajinga, na wapumbavu. Mnapaswa kuanza kutafuta. Fuatilia kwa ujasiri! Fungueni tu nyoyo zenu na mniruhusu Niishi ndani yenu. Tahadharini na muwe macho! Watu wengine katika kanisa ni wadanganyifu na mnapaswa kutilia mkazo sana maneno haya kila mara, maisha yenu yasije yakaathiriwa au kupata hasara fulani. Ondoa wasiwasi, mradi una ujasiri wa kusimama na kuzungumza kwa ajili Yangu, Nitachukua mzigo wa yote na kukupa uwezo! Mradi unauridhisha moyo Wangu, Nitakuonyesha tabasamu Yangu na mapenzi Yangu kila mara. Mradi una ujasiri na unaishi kwa kudhihirisha tabia ya mtoto wa kiume, Nitakuunga mkono na kukuweka katika nafasi muhimu. Unapokuja mbele Yangu, songa tu karibu na Mimi. Usiogope ikiwa huwezi kuzungumza. Mradi una moyo wa kutafuta, Nitakupa maneno. Sihitaji maneno matamu au kurai kwako; Ninachukia kitu cha aina hii zaidi ya vyote. Namchukia mtu wa aina hiyo zaidi ya wote. Yeye ni kama kipande cha kitu katika jicho Langu au mwiba katika mwili Wangu ambao lazima uondolewe. Vinginevyo wanangu hawawezi kutawala kwa ajili Yangu na watakuwa chini ya udhibiti wa kukaba. Kwa nini Nimekuja? Nimekuja kuwasaidia na kuwatia moyo wana Wangu, ili kwamba siku zao za kuvumilia ukandamizaji, unyanyasaji, ukatili, na dhuluma zitatoweka milele!

Kuwa jasiri. Nitatembea na wewe siku zote, Niishi na wewe, Nizungumze na wewe na Nitende nawe. Usiogope. Usisite kuzungumza. Daima ninyi ni wenye hisia, waoga, na wenye hofu. Wale ambao hawana faida yoyote kwa ujenzi wa kanisa lazima waondolewe. Hii ni pamoja na wale walio kanisani ambao hali zao si nzuri na wale ambao hawawezi kutenda kulingana na maneno Yangu, sembuse mama na baba yenu wasioamini. Sitaki mambo hayo. Lazima waondolewe, na asibaki hata mmoja. Fungua tu pingu zilizo kwenye mikono na miguu yako. Mradi unachunguza nia zako mwenyewe na hazihusiani na faida na hasara, wala kwa ajili ya umaarufu na utajiri, wala kwa ajili ya mahusiano ya kibinafsi, basi Nitaandamana na wewe, Nikuonyeshe mambo na kukupa mwongozo ulio wazi wakati wote.

Wanangu! Niseme nini? Ingawa Ninasema mambo haya, ninyi bado hamuufikirii moyo Wangu na bado ni waoga sana. Mnaogopa nini? Kwa nini bado mmefungwa kwa sheria na masharti? Nimewaachilia huru, lakini bado hamna uhuru. Kwa nini ni hivi? Wasiliana na Mimi zaidi na Nitakwambia. Usinijaribu. Mimi ni halisi. Sina udanganyifu, na vyote ni halisi! Kile Ninachosema ni kweli nami Sivunji ahadi Yangu kamwe.

Sura ya 44

Mimi ni mwenye haki, Mimi ni mwaminifu, Mimi ndimi Mungu anayechunguza moyo wa ndani zaidi wa mwanadamu! Nitafichua mara moja aliye wa kweli na aliye wa uongo. Hakuna haja ya kuwa na hofu, vitu vyote hufanya kazi kwa wakati Wangu. Ni nani asiyenitaka Mimi kwa dhati, ni nani asiyenitaka Mimi kwa dhati—Nitawaambia. Kuleni tu vizuri, kunyweni vizuri, njoo mbele Yangu na Nikaribieni nami Nitafanya kazi Yangu Mwenyewe. Msiwe na hamu sana ya matokeo ya haraka, kazi Yangu si kitu ambacho kinaweza kufanywa mara moja. Ndani yake kuna hatua Zangu na hekima Yangu, hivyo hekima Yangu inaweza kufichuliwa. Nitawawezesha kuona ni nini kinachofanywa kwa mikono Yangu—kuadhibu uovu na kuzawadia mema. Mimi hakika Simpendelei mtu yeyote. Ninakupenda kwa dhati wewe unayenipenda kwa dhati, na ghadhabu Yangu daima itakuwa pamoja na wale wasionipenda kwa dhati, ili kwamba waweze kukumbuka daima kwamba Mimi ni Mungu wa kweli, Mungu anayechunguza moyo wa ndani zaidi wa mwanadamu. Usitende kwa njia moja mbele ya wengine na utende kwa namna nyingine bila wao kufahamu; Ninaona wazi kila kitu unachofanya na ingawa unaweza kuwadanganya wengine huwezi kunidanganya Mimi. Ninaona yote waziwazi. Haiwezekani kwako kuficha chochote; vyote vimo mikononi Mwangu. Usifikiri kuwa wewe ni mjanja sana, kwa kufanya hesabu zako ndogondogo zikufaidi. Nakwambia: Haijalishi mwanadamu anaweza kubuni mipango kiasi kipi, iwe elfu kadhaa ama elfu nyingi, mwishowe hawezi kuepuka kutoka kwenye kiganja cha mkono Wangu. Vitu na matukio yote huendeshwa katika mikono Yangu, sembuse mtu mmoja! Usijaribu kuepuka au kujificha, usijidanganye au kuficha. Je, huwezi kuona kwamba uso Wangu mtukufu, hasira Yangu na hukumu Yangu imefichuliwa hadharani? Nitahukumu mara moja na bila huruma wale wote ambao hawanitaki Mimi kwa dhati. Huruma Yangu imefika mwisho na hakuna tena iliyobaki. Usiwe mnafiki tena na acha njia zako za kishenzi.

Mwanangu, tahadhari; tumia muda zaidi mbele Zangu nami Nitakuwa msaada wako. Usiogope, toa upanga Wangu mkali ukatao kuwili, na—kulingana na mapenzi Yangu nami—pigana na Shetani mpaka mwishoni, Nitakulinda; usiwe na wasiwasi. Mambo yote yaliyofichwa yatafunguliwa na kufichuliwa. Mimi ni Jua ambalo linatoa nuru, likimulika giza lote bila huruma. Hukumu Yangu imeshuka kabisa na kanisa ni uwanja wa vita. Nyote mnapaswa kuwa tayari na mnapaswa kutoa nafsi zenu zote kwa vita vya mwisho vya uamuzi; Mimi hakika Nitakulinda ili uweze kunipigania vita vizuri, vya ushindi.

Kuwa makini, mioyo ya watu leo ni yenye udanganyifu na haitabiriki na hawapaswi kuaminiwa. Ni Mimi tu Niliye upande wako kabisa. Hakuna udanganyifu ndani Yangu; Niegemee Mimi tu! Hakika wana Wangu watashinda katika vita vya mwisho vya uamuzi na bila

shaka Shetani atajitokeza na kushambulia katika uchungu wake wa kifo. Usiogope! Mimi ni nguvu yako, Mimi ni kila kitu chako. Usifikiri juu ya mambo mara kwa mara, huwezi kushughulikia mawazo mengi sana. Nimesema hapo awali, Sitawavuta tena katika njia kwa kuwa hakuna muda wa kupoteza hata kidogo. Sina wakati wa kuwahitaji msikilize kwa makini tena na kuwakumbusha—haiwezekani! Malizeni tu maandalizi yenu kwa ajili ya vita. Mimi nakuwajibikia kikamilifu; vitu vyote viko mikononi Mwangu. Hivi ni vita vya kufa na kupona na yatakuwa mapambano ya kufa na kupona. Lakini unapaswa kutambua kwamba Mimi ni mshindi milele na Asiyeshindwa, na kwamba Shetani bila shaka ataangamia. Hii ni mbinu Yangu, kazi Yangu, mapenzi Yangu na mpango Wangu!

Imekamilika! Yote yamekamilika! Usiwe mwoga au mwenye hofu. Mimi pamoja na wewe na wewe pamoja na Mimi tutakuwa wafalme milele na milele! Maneno ambayo Nimesema hayatabadilika milele na matukio yatawafika hivi karibuni. Kesheni! Mnapaswa kutafakari vizuri kila neno; msiwe na mashaka kuyahusu tena. Lazima muwe wazi kuyahusu! Kumbuka—tumia muda zaidi mbele Zangu!

Sura ya 45

Mnawahukumu ndugu zenu hadharani kana kwamba si kitu. Hakika hamjui mema na maovu; hamna aibu! Je, hii si tabia mbaya ya kifidhuli, ya kutojali? Kila mmoja wenu amechanganyikiwa na ni mwenye moyo mzito; mnabeba mizigo mingi na hakuna sehemu Yangu ndani yako. Watu vipofu! Ninyi ni wakatili namna gani—hili litakoma lini?

Nazungumza nanyi kutoka moyoni Mwangu mara kwa mara na Ninawapa kila kitu Nilicho nacho, lakini ninyi ni wachoyo sana na hamna ubinadamu hata kidogo; hili kweli ni jambo lisiloeleweka. Kwa nini mnashikilia dhana zenu wenyewe? Kwa nini huwezi kuniruhusu Niwe na sehemu kidogo ndani yako? Ningewezaje kuwadhuru? Hampaswi kuendelea kutenda kwa njia hii—hakika siku Yangu haiko mbali na sasa. Msizungumze ovyo ovyo, kutenda kiholela, au kupigana na kusababisha shida; hili lina faida gani katika maisha yenu? Ninawaambieni kwa kweli, hata kama hakuna mtu hata mmoja atakayeokolewa siku Yangu itakapowadia, bado Nitaendelea kushughulikia masuala kulingana na mpango Wangu. Lazima mjue kwamba Mimi ni Mwenyezi Mungu! Hakuna kitu, hakuna mtu, hakuna tukio linalojaribu kuzuia hatua Zangu kwenda mbele. Hampaswi kufikiri kwamba Sina njia ya kutekeleza mapenzi Yangu bila ninyi. Naweza kukwambia kwamba ukiyachukulia maisha yako mwenyewe kwa namna hii hasi, utayaangamiza maisha yako mwenyewe tu na haitakuwa shida Yangu.

Kazi ya Roho Mtakatifu imeendelea hadi hatua fulani na ushuhuda umefikia kilele. Huu ni ukweli ulio wazi. Harakisheni, fungueni macho yenu yasiyoona vizuri, msiruhusu jitihada Zangu

za bidii ndani yenu ziwe bure, na msijiingize katika raha tena. Mnafurahia kufanya matendo mema mbele Yangu, lakini wakati Sipo matendo yenu na tabia zenu vinaweza kuinuliwa mbele Zangu ili Nione? Hamjui tofauti kati ya mema na maovu! Ninyi hamnisikilizi, mnafanya jambo moja mbele Yangu na lingine wakati Siko. Bado hamjagundua kwamba Mimi ni Mungu ambaye Anaangalia kwa kina ndani ya moyo wa mwanadamu. Wajinga mlioje!

Baadaye, katika njia iliyo mbele, hampaswi kusababisha ulaghai au kushiriki katika udanganyifu na upotovu, vinginevyo matokeo yatakuwa yasiyofikirika! Bado hamwelewi udanganyifu na upotovu ni nini. Matendo yoyote au tabia ambazo hamwezi kuniruhusu Nione, ambazo hamwezi kuziweka hadharani ni udanganyifu na upotovu. Sasa mnapaswa kuelewa hili! Mkishiriki katika udanganyifu na upotovu katika siku zijazo, msijifanye kuwa hamwelewi, huko ni kufanya tu makosa kwa makusudi, kuwa na hatia hata zaidi. Hii itawasababisha tu kuteketezwa na moto, au hata mambo yakiwa mabaya zaidi, kujiangamiza. Lazima muelewe! Kile mnachokabiliwa nacho leo ni kuadibu kwa upendo; bila shaka si hukumu ya kikatili. Kama hamwezi kuona hili, basi ninyi ni wa kusikitisha sana, na ninyi hamna matumaini kabisa. Kama hamko tayari kukubali kuadibu kwa upendo, basi yanayoweza kuwapata tu ni hukumu ya kikatili. Jambo hilo litakapotokea, msilalamike kwamba Sikuwaambia. Si Mimi niliyekwepa majukumu Yangu bali ni nyinyi ambao hamjasikiliza maneno Yangu na hamjatekeleza maneno Yangu. Ninawaambia hili sasa, Nisije Nikalaumiwa baadaye.

Sura ya 46

Yeyote anayejitumia na kujitolea kwa uaminifu kwa ajili Yangu, hakika Nitakuinga mpaka mwisho kabisa; mkono Wangu hakika utakushikilia ili kwamba daima una amani na mwenye furaha daima na kila siku una mwanga Wangu na ufunuo. Hakika Nitakupa baraka Zangu mara dufu, ili uwe na kile Nilicho nacho na umiliki kile Nilicho. Kile unachopewa ndani yako ni maisha yako, na hakuna mtu anayeweza kukichukua kutoka kwako. Usijiletee taabu au kufadhaika; ndani Yangu kuna amani na furaha tu. Ninakupenda kwa dhati, wewe mtoto ambaye hunisikiza kwa dhati na kunitii. Wale ambao Ninawachukia zaidi ni wanafiki na hakika Nitawaangamiza. Nitaondoa dalili yoyote ya ulimwengu kutoka kwa nyumba Yangu, na kuondosha vitu vyote ambavyo Siwezi kuvumilia kuona.

Ndani ya moyo Wangu Najua hasa nani ambaye ananitaka kwa dhati na ni nani ambaye hanitaki. Wanaweza kujificha vizuri na kuweka kisingizio kijanja, na inaweza hata kusemwa kuwa wao ni waigizaji bora zaidi duniani, lakini Naona wazi kila kitu wanachoshikilia ndani ya mioyo yao. Usidhani kuwa Sijui yaliyo ndani ya moyo wako; kwa kweli hakuna mtu anayeelewa wazi zaidi kuliko Mimi. Najua kilicho moyoni mwako; wewe uko tayari kujitoa kwa ajili ya Mungu, kutumia kwa ajili ya Mungu, ni kwamba tu hutaki kutumia mazungumzo mazuri ili

kuwafanya wengine wafurahie. Ona wazi! Ufalme wa leo haujengwi kwa nguvu za mwanadamu, lakini utajengwa kwa ufanisi kikamilifu kwa kutumia hekima Yangu nyingi na jitihada ya bidii. Yeyote aliye na hekima na anayemiliki kile Nilicho ndani yake atashiriki katika ujenzi wa ufalme. Usiwe na wasiwasi tena, wewe daima huwa na wasiwasi mwingi sana, bila kujali ufunuo au nuru ya mapenzi Yangu ndani yako. Usifanye hivyo tena. Fanya ushirika zaidi na Mimi kuhusu jambo lolote ili kuepuka mateso kutoka kwa matendo yako mwenyewe.

Labda kwa juu inaonekana kama Mimi ni vuguvugu kwa kila mtu, lakini je, unajua kile Ninachofikiria ndani? Mimi daima Ninawainua wanyenyekevu juu kabisa, na daima Ninawaleta chini wale ambao wanajipenda, wanaojikweza. Wale wasioelewa mapenzi Yangu watapoteza sana. Lazima ujue kwamba hiki ndicho Nilicho, ni tabia Yangu—hakuna anayeweza kukibadilisha, hakuna mtu anayeweza kukielewa vizuri. Ni kwa njia ya ufunuo Wangu tu ndiyo unaweza kuelewa, vinginevyo hutakielewa vizuri kabisa pia; usiwe mwenye kiburi. Ingawa watu wengine wanaweza kuzungumza vizuri, mioyo yao huwa sio ya uaminifu Kwangu kamwe, daima kunipingana kisiri; Nitamhukumu mtu wa aina hii.

Usilenge tu kufuata nyayo za wengine, unapaswa kuzingatia mwelekeo Wangu na tabia Yangu. Ni kwa njia hii tu ndiyo hatua kwa hatua utapata kuelewa mapenzi Yangu; vitendo vyako basi vitapatana na mapenzi Yangu na hutafanya makosa. Usilie wala kuwa na huzuni; Naona wazi kila kitu unachofanya, tabia yako yote na yote unayofikiria, na Ninajua matakwa yako na matamano yako ya dhati; Nitakutumia wewe. Sasa ni wakati muhimu, wakati wa kukujaribu umefika. Je, bado hujaona? Je, bado hajatambua? Kwa nini Nachukua mtazamo kama huu kwako? Je, unajua? Nimekufichulia mambo haya na wewe una ufahamu mdogo. Lakini usiache—endelea kukazana na kuingia kwako na Nitaendelea kukupa nuru. Je, umegundua kwamba kadiri unavyotii na kunisikiza zaidi, ndivyo unavyong’aa zaidi ndani na ndivyo unavyokuwa na ufunuo zaidi ndani? Na ndivyo unavyokuwa na maarifa zaidi kunihusu na ndivyo unavyopata uzoefu zaidi? Usishikilie kwa uthabiti kila mara dhana zako mwenyewe kwani kufanya hivi kutaziba mtiririko wa maji Yangu ya uhai na kuzuia kutekelezwa kwa mapenzi Yangu. Lazima ujue kwamba kumpata mtu mmoja kikamilifu si jambo rahisi. Usifikiri kwa njia ya utata. Fuata tu, na usifikirie tena!

Sura ya 47

Mwenyezi Mungu mwenye haki—mwenye Uweza! Ndani Yako hakuna chochote kabisa kilichofichwa. Kila fumbo tangu zamani hadi milele, ambalo halijawahi kufumbuliwa na binadamu, ndani Yako linadhihirika na kwa jumla kuwa wazi. Hatuhitaji tena kutafuta na kupapasa, kwa maana leo nafsi Yako inadhihirika wazi kwetu, Wewe ndiye fumbo ambalo limefichuliwa, Wewe ni Mungu wa vitendo Mwenyewe; kwa kuwa leo Umekuja uso kwa uso na

sisi, na tuionapo nafsi Yako, tunaona kila fumbo la ulimwengu wa kiroho. Kweli hiki ni kitu ambacho hakuna mtu angeweza kuwaza! Wewe uko miongoni mwetu leo, hata ndani yetu, karibu sana nasi; haliwezi kuelezeka! Fumbo lililo ndani ya hili ni lisilo na kifani!

Mwenyezi Mungu amekamilisha mpango Wake wa usimamizi. Yeye ndiye Mfalme mshindi wa ulimwengu. Vitu vyote na mambo yote yanadhibitiwa mikononi Mwake. Watu wote wanapiga magoti katika ibada, wakiliita jina la Mungu wa kweli—Mwenyezi. Kwa maneno kutoka katika kinywa Chake, mambo yote yanafanyika. Kwa nini ninyi ni wazembe sana, msiweze kujielekeza kwa bidii kufanya kazi pamoja na Yeye, kujiunga kwa karibu na Yeye, na kwenda na Yeye katika utukufu? Inawezekana kuwa mko tayari kuteseka? Mko tayari kutupwa nje? Je, ninyi mnafikiri kwamba Sijui ni nani anayejitolea kwa dhati Kwangu, na ni nani ambaye amejitumia kwa dhati kwa ajili Yangu? Ujinga! Wapumbavu! Hamwezi kufahamu nia Zangu, na sembuse kuweza kuidhukuru mizigo Yangu, daima mkinifanya Niwe na wasiwasi kuwahusu, daima mkinifanya nijitahidi kwa ajili yenu. Je, hili litaisha lini?

Kuishi kwa kunidhihirisha Mimi katika kila kitu, kunishuhudia katika kila kitu—je, kufanya hivyo sit u jambo la kufungua midomo yenu na kutunga maneno machache pamoja? Hamjui tofauti kati ya mema na maovu! Hamko na Mimi katika kile mnachofanya, na sembuse Mimi kuwepo katika maisha yenu ya kila siku. Najua kuwa ninyi hamchulii kumwamini Mungu kuwa jambo la uzito, hivyo haya ndiyo matunda mnayozaa! Bado hamko macho, na mkiendelea hivi, mtaliaibisha jina Langu.

Jiulize, unapozungumza, je, Niko pale na wewe? Unapokula au kuvaa nguo zako, je, kuna ahadi Yangu hapo? Kweli, ninyi ni msiojali! Kila wakati ambapo matatizo yako hayakemewi moja kwa moja, basi unaonyesha jinsi ulivyo kweli, na hakuna yeyote kati yenu aliye msikivu. Isingekuwa hivyo, ninyi mngejiona kuwa wakuu na kufikiri kwamba mnamiliki vitu vingi ndani yenu. Je, hamjui kuwa ndani yenu, kilichowajaza ninyi, ni sura ya uovu ya Shetani? Fanyeni kazi na Mimi ili kumwaga vitu hivi vyote nje. Acha kile Nilicho na kile Nilicho nacho kikae ndani yako kabisa; ni hivyo tu ndivyo unaweza kuishi kwa kunidhihirisha Mimi, unishuhudie kwa uhalisi zaidi, na muwe sababu inayowafanya watu zaidi watii mbele ya kiti Changu cha enzi. Lazima mjue mzigo ulio mabegani mwenu ni mzito kiasi gani: kumtukuza Kristo, kumdhihirisha Kristo, kumshuhudia Kristo, ili watu wengi wapate wokovu kwamba ufalme Wangu uweze kusalia imara na usiotikisika. Ninataja haya yote ili kwamba msiboronge tu, bila ya kuelewa umuhimu wa kazi ya leo.

Kutojiweza mnapokabiliwa na matatizo, kama siafu kwenye kikaango kimoto, wakizunguka huku na kule: hii ndiyo tabia yenu. Kwa nje, mnaonekana kama watu wazima, lakini maisha yenu ni yale ya mtoto; kile mnachojua kufanya ni kusababisha usumbufu tu na kuongezea juu ya

mzigo Wangu. Ikiwa kuna kitu kidogo zaidi ambacho Sijishughulishi nacho, ninyi husababisha usumbufu. Je, hilo si kweli? Msiwe wenye kujidai. Ninachosema ni ukweli. Msifikirie daima kwamba daima Ninawakaripia bila kukoma, kana kwamba Nilikuwa natumia maneno ya kifahari tu; hii ndiyo hali yenu halisi.

Sura ya 48

Mimi nina wasiwasi, lakini wangapi kati yenu wanaweza kuwa na nia moja na mawazo sawa na Mimi? Ninyi hamyasikilizi tu maneno Yangu, mkipuuza kabisa na kushindwa kuyatilia maanani, badala yake mkizingatia tu mambo yenu wenyewe ya juu juu. Mnachukulia kujali Kwangu kwa bidii na juhudi kama jitihada za bure; je, dhamiri yenu haiwahukumu? Ninyi ni wajinga na hamna mantiki; ninyi ni wapumbavu, na hamwezi kuniridhisha kabisa. Niko upande wenu kabisa—ninyi mnaweza kuwa upande Wangu kiasi gani? Mmeelewa visivyo nia Yangu, na hakika huu ni upofu wenu na kutoweza kuona mambo, daima mkinifanya Niwe na wasiwasi kuwahusu na kutumia muda kwenu. Sasa, ni kiasi gani cha muda wenu ambao mnaweza kuutumia na kutenga kwa ajili Yangu? Mnapaswa kujiuliza zaidi.

Nia Yangu yote ni kwa sababu yenu—je, mnaelewa hili kweli? Kama kweli mngeelewa, mngekuwa mmekwisha kufahamu nia Yangu na kuufikiria mzigo Wangu. Msiwe wazembe tena, la sivyo Roho Mtakatifu hatafanya kazi ndani yenu, jambo ambalo litazifanya roho zenu zife and kuanguka kuzimuni. Je, hilo si jambo baya sana kwako? Hakuna haja ya Mimi kuwakumbusha tena. Mnapaswa kuchunguza dhamiri zenu na kujiuliza: Je, ni kwamba Ninawahurumia sana, au kwamba ninyi mna madeni Yangu mengi sana? Msichanganye mema na mabaya na muwe bila akili! Sasa si wakati wa kupigania nguvu na faida au kushiriki katika kula njama, badala yake lazima muweke kando kwa haraka mambo haya ambayo ni yenye kuleta madhara kwa maisha na kutafuta kuingia ndani ya ukweli. Ninyi ni wazembe sana! Hamwezi kuuelewa moyo Wangu au kutambua nia Yangu. Kuna mambo mengi ambayo Sikupaswa kuyasema, lakini ninyi ni watu mlionchanganyikiwa sana ambao hamwelewi, imenibidi Niyaseme mara kwa mara, na hata hivyo, ninyi bado hamjauridhisha moyo Wangu.

Nikiwahesabu mmoja mmoja, ni wangapi wanaoweza kuufikiria moyo Wangu kwa hakika?

Sura ya 49

Ili kutumikia kwa uratibu, mtu lazima ajiunge kwa usahihi, na pia awe mchangamfu na dhahiri. Zaidi ya hayo, mtu lazima awe na uchangamfu, nguvu, na kujawa na imani, ili kwamba wengine waruzukiwe na watakuwa wakamilifu. Kunitumikia Mimi lazima utumikie Ninayonua, sio tu kuupendeza moyo Wangu, lakini zaidi ya hayo kuridhisha nia Zangu, ili Niridhishwe na kile Ninachotimiza ndani yako. Jaza maisha yako na neno Langu, jaza usemi Wako na nguvu

Yangu, hili ndilo Ninalohitaji kutoka kwako. Je, kufuata tamaa zako mwenyewe kunafichua mfano Wangu? Je, hilo litauridhisha moyo Wangu? Je, wewe ni mtu ambaye amechunguza nia Zangu kwa dhiti? Je, wewe ni mtu ambaye amejaribu kwa kweli kuuelewa moyo Wangu? Je, wewe hakika umejitoe mwenyewe kwa ajili Yangu? Je, umejitumia mwenyewe kwa ajili Yangu? Je, umetafakari juu ya maneno Yangu?

Mtu lazima atumie hekima katika kila kipengele na kutumia hekima kutembea katika njia Yangu kamili. Wale wanaotenda kulingana na neno Langu ni wenye busara zaidi kuliko wote na wale wanaotenda kulingana na neno Langu ndio watiifu zaidi. Ninachosema kinakuwa na huhitaji kujadili na Mimi au kujaribu kunishawishi. Kila kitu Ninachosema Ninasema nikiwa na wewe akilini (bila kujali kama mimi ni mkali au mpole), ukilenga kuwa mtiifu hilo litakuwa jambo zuri, na hii ndiyo njia ya hekima ya kweli (na ya kuzuia hukumu ya Mungu kukupata). Siku ya leo, ndani ya nyumba Yangu, usiwe na heshima mbele Yangu na kusema mambo mengine nyuma Yangu. Nataka uwe wa utendaji; huhitaji kutumia maneno ya kuvutia. Kwa wale ambao ni wa utendaji, kuna kila kitu. Kwa wale ambao sio, hakuna kitu. Hata mwili wao utarejeshwa kwa kutokuwepo pia, kwa sababu bila utendaji, kuna utupu tu; hakuna maelezo mengine.

Katika imani yenu katika Mungu, Ningewataka muwe wenye bidii na msifikirie kile mtakachonufaika nacho au kupoteza, wala kwa yote mliyo nayo; mnapaswa kutafuta tu kuweka miguu yenu katika njia ya kweli, na msitingike kwa ajili ya mtu yeyote au kudhibitiwa na mtu yeyote. Hii ndiyo inayojulikana kama kuwa nguzo ya kanisa, mshindi wa ufalme, lakini kufanya vinginevyo kunamaanisha wewe hustahili kuishi mbele Yangu.

Hali zinaweza kutofautiana, kama vile njia za kuwa karibu na Mimi. Watu wengine hupenda kusema maneno yanayosikika kuwa mazuri na kutenda kwa njia ya ibada mbele Yangu. Hata hivyo, nyuma ya matukio wao wamevurugika kabisa na maneno Yangu hayapo kabisa katika yale wanayoyatenda. Wao ni wa kuchukiza na wa kukasirisha; haiwezekani kwamba wangeweza kumletea mtu ujenzi wa maadili au kuwa na kitu cha kuruzuku. Ninyi hamwezi kuuzingatia moyo Wangu na hiyo ni kwa sababu tu hamwezi kuwa na ukaribu zaidi au kushiriki na Mimi, ninyi huniacha daima Niwe na wasiwasi na kufanya kazi kwa bidii kwa niaba yenu.

Sura ya 50

Makanisa yote na watakatifu wote wanapaswa kutafakari kuhusu siku zilizopita na kutumainia siku za usoni. Ni mangapi kati ya matendo yenu ya zamani ndiyo yanayostahili, na ni mangapi kati yao yalishiriki katika ujenzi wa ufalme? Usiwe mtu mwenye kujifanya kujua kila kitu! Unapaswa kuona wazi dosari zako na unafaa kuelewa hali zako mwenyewe. Najua kwamba

hakuna yeyote kati yenu yuko tayari kuweka jitihada yoyote na kugharimika muda wowote kuhusu hili, kwa hivyo hamuwezi kupata ujuzi wowote. Mnaharibu muda wenu wote katika kula, kunywa na kustarehe. Wakati wachache wenu wanakuja pamoja mnafanya mchezo, bila kuwa makini kushiriki mambo ya kiroho maishani au kutoa maisha nyinyi kwa nyinyi. Siwezi kustahimili kuwaona mkicheka na kufanya mzaha mnapozungumza, ilhali nyinyi ni wapumbavu sana. Nimesema mara nyingi, lakini hamjui tu maana ya kile Ninachosema—je, hili si jambo ambalo liko wazi kabisa kwamba liko dhahiri kabisa kwenu? Nimesema mambo kama haya awali lakini bado hamjaridhishwa na hamkubali kile Ninachosema, mkifikiri kwamba Siwaelewi, mkifikiri kwamba kile Ninachosema sio halisi. Au yaweza kuwa kwamba hii sivyo ilivyo?

Ukishughulika na Mimi kwa uzembe basi nitakuweka upande mmoja. Wewe thubutu tu kuwa mzembe tena! Wewe thubutu tu kuwa mzembe na mvivu tena! Maneno Yangu ni kisu kinachochonga; chochote kisichopatana na mapenzi Yangu kitakatwa na kisu hiki, na hufai kuwa na nadhari sana kuhusu kujiheshimu. Ninakuchonga ili uweze kupata umbo na kufuata mapenzi Yangu. Usikose kuuelewa moyo Wangu; njia ya pekee inayokubalika ni kwa wewe kuwa mwenye kuujali moyo Wangu kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo. Ukionyesha kujali hata chembe, Mimi sitageuka mbali na wewe kwa dharau. Usilipuuze bila kufikiri kila mara; yaruhusu mapenzi Yangu siku zote yafanyike kwako.

Majeshi ya watakatifu yote yako katika nafasi tofauti, kwa hivyo bila shaka nyote mko na kazi tofauti. Lakini mnapaswa kufanya kila kitu katika uwezo wenu kugharimika kwa kweli kwa ajili Yangu, na wajibu wenu ni kufanya kila mnaloweza. Mnapaswa kuwa waaminifu katika hili, muwe na hiari kwa furaha, na kwa kweli ni sharti msiwe shingo upande. Vinginevyo, hukumu Yangu daima itakuwa juu yenu, miili yenu, roho na nafsi havitaweza kuistahimili, na kutakuwa na kulia na kusaga meno.

Sura ya 51

Ee! Mwenyezi Mungu! Amina! Ndani Yako yote yanaachiliwa, yote ni huru, yote ni wazi, yote hufichuliwa, yote hung'aa, bila sitara au maficho yoyote. Wewe ni Mwenyezi Mungu mwenye mwili. Umetawala kama Mfalme. Umefichuliwa wazi, wewe tena si fumbo lakini Umefichuliwa kabisa milele na milele! Kwa kweli Nimefichuliwa kabisa, Nimefika hadharani, na Nimejitokeza kama Jua la haki kwa kuwa leo si enzi ya kuonekana kwa nyota ya asubuhi tena, si awamu ya sitara tena. Kazi Yangu ni kama mwanga wa umeme; inakamilishwa kwa upesi kama mpigo wa radi. kazi Yangu imeendelea hadi hatua hii na yeyote anayekawia au kuzembea anaweza tu kukabiliwa na hukumu isiyo na huruma. Ni lazima uelewe dhahiri hasa kwamba Mimi ni uadhama na hukumu na Mimi si huruma na upendo tena kama mnavyodhani. Kama bado huelewi vizuri hoja hii, kile utakachopokea basi ni hukumu, kwa kuwa wewe

mwenyewe utaonja kile ambacho wewe bado hujakiri, vinginevyo bado utakuwa na mashaka na kutothubutu kuwa imara katika imani yako.

Kile ambacho Nimewaaminia, mna uwezo wa kukimaliza kwa mapenzi? Nasema kwamba inahitaji hekima kufanya kitu chochote, ilhali ni vitu vingapi mmefanya ambavyo mmechunguza kwa makini ushawishi Wangu mara kwa mara, na kuvipa fikira zaidi? Hata kama mnao ufahamu wa neno moja la ushawishi Wangu na mnafikiri ni sawa mnapolisikia, hatimaye si la muhimu kwenu. Mnapolisikia, mnalielekeza kwa hali zenu halisi wenyewe na kujichukia. Lakini baadaye mnaliamini kuwa jambo dogo.. Suali leo ni kama maisha yako yanaweza kuendelea au la; si suali la jinsi ambao wewe umerembeka kwa nje. Hakuna kati yenu aliye na azimio lolote na hamko tayari kuwa na ushupavu, hamtamani kulipa gharama, hamtaki kuweka kando anasa zisizodumu za dunia na bado mnahofia kupoteza baraka kutoka mbinguni, huyu ni mtu wa aina gani? Huyu ni mjinga! Hampaswi kuhisi kukerwa—je, kile ambacho Nimesema si cha kweli? Je, hakijasitiza kile ambacho umekifikiri kwako mwenyewe? Wewe huna ubinadamu! Wewe huna hata sifa ya mtu wa kawaida, na hata kama hivi ndivyo kulivyo, bado wewe hujioni mwenyewe kama maskini, wewe ni taratibu na asiyejali siku yote nzima, wa kujiridhisha! Wewe hujui jinsi upungufu wako mwenyewe ni mkubwa na kile unachokosa. Upumbavu ulioje!

Je, hamwoni kwamba kazi Yangu tayari ishakuja hadi mahali kama hapo? Mapenzi Yangu yote yako ndani yenu, mtaweza kuyafahamu lini, mtafikiri kuyahusu lini? Mzembe! Wewe huko tayari kulipa gharama, huko tayari kufanya kazi ngumu, huko tayari kuchukua wakati, na huko tayari kuweka bidii. Acha Nikwambie! Kadiri unavyohofia kupata taabu, ndivyo maisha yako yatakavyokuwa na faida chache zaidi, aidha ndivyo utakavyokabiliwa na vikwazo zaidi maisha yako yanavyokua, na ndivyo uendeleaji wake unaonekana hutaendelea zaidi. Nakukumbusha mara nyingine tena (Sitalisema tena)! Yeyote asiyewajibika na maisha yake mwenyewe, Mimi sitamjali na Nitamwacha. Tayari Nimeshaanza kulitekeleza hili; hujaona hili kwa uwazi? Haya si mapatano ya kibiashara wala si ubadilishanaji na ugawaji wa bidhaa, lakini ni maisha, je hilo ni dhahiri?

Sura ya 52

Ninatokea kama Jua la haki, na nyinyi pamoja na Mimi tunashiriki utukufu na baraka nzuri, milele na milele! Huu ni ukweli thabiti, na tayari umeanza kutimizwa kwenu. Kwa yote ambayo Nimewaahidi, Nitawatimizia; yote Nisemayo ni ya kweli, na hayatarudi tupu. Baraka hizi nzuri ziko juu yenu, hakuna yeyote mwingine anayeweza kuzidai; ni matunda ya utumishi wenu kwa kukubaliana na Mimi kwa maafikiano. Zitupilie mbali dhana zenu za kidini; yaamini maneno Yangu kuwa ya kweli na msiwe mwenye shaka! Mimi sifanyi utani na nyinyi, Namaanisha Ninayoyasema; wale ambao Nawakirimu baraka ndio wanaozipokea; wale ambao Siwatawazi

baraka hawazipokei; hili linaamuliwa na Mimi. Baraka nzuri ya kidunia ni nini? Kwa mtazamo Wangu si kitu ila kinyesi cha mnyama, yenye thamani chini ya senti. Kwa hivyo msizithamini sana starehe za kidunia; si kufurahia baraka za mbinguni na Mimi ni ya maana zaidi, kitu cha thawabu zaidi?

Awali ukweli haukuwa umefunuliwa, na Mimi Sikuwa Nimeonekana waziwazi; nyinyi mlinishuku Mimi na hamkuthubutu kuwa wenye uhakika kunihusu. Hata hivyo, sasa mambo yote yamefunuliwa, na Nimejitokeza kama Jua la haki; kama bado mko katika shaka, mnasema nini kuhusu hilo? Wakati giza lilipofunika dunia, ya kwamba hamkuweza kuuona mwanga iliweza kusamehewa, lakini sasa jua limeangaza pembe zote zenye giza; yalilofichwa hayajafichika tena, yaliyosetiriwa hayajasetiriwa tena; kama bado mko na shaka, basi Sitawasamehe kwa urahisi! Sasa ni wakati wa kuwa na uhakika kabisa kunihusu, wakati wa kuwa tayari kujitolea Kwangu na kugharimika kwa ajili Yangu. Yeyote anayenipinga kwa njia yoyote ndogo ile atashambuliwa mara moja kwa mioto ya hukumu bila kuwaza tena au kusita. Kwani sasa ni wakati ambao hukumu isiyo na huruma imefika; kwa kuwa wale ambao fikra na mioyo yao si minyofu, kutakuwa na hukumu ya papo hapo; hii ni maana ya kweli ya “Kazi Yangu ni kama mwako wa ghafla wa umeme” kama ilivyozungumziwa.

Inafanyika kwa haraka; haina budi ila kuwastaajabisha watu, itawatia watu hofu, haiwezi kucheleweshwa tena na haiwezi kuzuiliwa. Kadri kazi Yangu inavyofanywa, ndivyo inavyosonga mbele kwa haraka; yeyote ambaye si mwangalifu na tayari siku zote huwa katika hatari ya kutelekezwa; kamwe msijaribu tena kujaribu moyoni mwako. Kazi Yangu imeanza kikamilifu, ikienea kwa mataifa yasiyo Uyahudi na ulimwengu dunia. Mioto ya hukumu ni katili na bila huruma au upendo kwa mtu yeyote. Wale ambao ni waaminifu kwa Mungu lakini bado wako na fikra na mawazo yasiyo sahihi, au hata wanapinga kidogo, watahukumiwa bila shaka. Yeyote ambaye mwanga Wangu unamwangazia ataishi ndani ya mwanga, na kutenda katika mwanga, na kunitumikia hadi mwisho wa barabara. Wale ambao hawaishi katika mwanga wanaishi gizani. Nitafanya uamuzi baada ya kuwahukumu, kulingana na msimamo wao kuhusu hatia yao.

Siku Yangu imefika, Siku Yangu iliyotajwa awali sasa iko mbele ya macho yenu, kwa kuwa nyinyi mnashuka pamoja na Mimi. Mimi na nyinyi, nyinyi na Mimi, tumekutana angani, tukishiriki utukufu pamoja. Siku Yangu kwa kweli imefika kabisa!

Sura ya 53

Mimi ndiye mwanzo, na Mimi ndiye mwisho. Mimi ndiye Mungu mmoja wa kweli aliyefufuka na kamili. Nasema maneno Yangu mbele yenu, na lazima muamini Ninachosema

kwa thabiti. Mbingu na dunia zinaweza kupita lakini hakuna herufi moja au mstari mmoja wa kile Ninachosema kitawahi kupita. Kumbuka hili! Kumbuka hili! Punde ambapo Nimesema, hakuna neno hata moja limewahi kurudishwa na kila neno litatimizwa. Sasa wakati umewadia na lazima muingie katika uhalisi kwa haraka. Hakuna muda mwingi. Nitawaongoza wana Wangu hadi katika ufalme mtukufu na kile ambacho mmejitahidia na kutamani sana kitafanikishwa. Wanangu! Inukeni haraka na mnifuate! Tayari hakuna muda wa ninyi kuwa mkilifikiri. Muda uliopotezwa hautarudi kamwe, baada ya giza kuna nuru, na unyakuzi uko mbele ya macho yenu. Je, mnaelewa? Fungueni macho yenu! Amkeni upesi! Hamruhusiwi sasa katika kuwasiliana miongoni mwenu kushiriki katika kupiga domo au kusema chochote kisicho cha maana katika ujenzi wa kanisa, kilicho cha muhimu ni kuwaruzuku ndugu na uzoefu wako wa utendaji au jinsi unavyoangazwa mbele ya Mungu na kujijua; yeyote anayeweza kutoa hili atakuwa na kimo! Sasa watu wengine hawaogopi, na bila kujali kile Ninachosema au kiasi gani Ninachokuwa na wasiwasi, bado hauogopi; nafsi yako nzee haijiruhusu kuguswa, kwa hivyo unaweza kuendelea kwa njia hii! Ona ni nani atakayeangamizwa! Daima unafikiri kuhusu kuishika dunia, ukitamani sana utajiri, na kuhisi uhusiano wa karibu sana na wana wako wa kike, wa kiume na mume wako. Haya, unaweza kuendelea kuhisi uhusiano wa karibu! Sio kwamba maneno Yangu hayajazungumzwa kwenu, na mnaweza kuendelea jinsi mnavyotaka! Katika siku za usoni za karibu mtalewa kila kitu, lakini mtakuwa mmechelewa sana tayari na yote yanayowangoja ni hukumu.

Sura ya 54

Ninalielewa kila kanisa kama kiganja cha mkono Wangu. Usifikiri kwamba Siko wazi au Sielewi. Ninawaelewa na kuwajua watu wote mbalimbali wa kila kanisa hata zaidi. Ninahisi hisia ya umuhimu kwamba ni lazima Nikufundishe. Nataka nikufanye ukue hadi utu uzima haraka zaidi ili siku ambayo utaweza kutumiwa na Mimi itakuja haraka zaidi. Nataka vitendo vyenu viwe vimejaa hekima Yangu ili muweze kumdhihirisha Mungu kila pahali. Kwa njia hii lengo Langu kuu litafanikishwa. Wanangu! Mnapaswa kuwa wenye kufikiria nia Zangu, msifanye Nishikilie mikono yenu Ninapowafundisha. Lazima mjifunze kujua nia Zangu, mjifunze kuona hadi kwenye kina cha mambo, kuwawezesha kushughulikia kila jambo linalowajia kwa urahisi na bila ugumu. Pengine katika mafundisho yenu, mara ya kwanza hamtaelewa, kisha mara ya pili, mara ya tatu.... Hatimaye mtalewa nia Zangu.

Maneno yenu kila mara huwa na sifa isiyoopenyeka, mfikiri wenyewe kuwa hii ni hekima, sivyo? Mara mkiwa wasiotii, na mara nyingine mkiwa wenye utani, wakati mwingine na mawazo au wivu wa mwanadamu.... Kwa jumla, mnazungumza bila uthabiti, msijue jinsi ya kuruzuku maisha kwa wengine au jinsi ya kufahamu hali zao, na kushiriki katika mawasiliano ya

kibwege. Fikira zenu haziko wazi, hamjui hekima ni nini, ujanja ni nini, ninyi mmechanganyikiwa sana tu. Mnachukulia ujanja na udanganyifu kama hekima, je, hili haliliaibishi jina Langu? Je, hili halinikufuru? Je, hili halileti mashtaka ya uwongo dhidi Yangu? Hivyo lengo mnalotafuta ni lipi? Je, mmefikiria kuhusu hilo? Je, mmejitahidi kufanya hili? Nakuambia, nia Zangu ni mwelekeo na lengo ambalo mnatafuta, vinginevyo, yote yatakuwa bure. Wale ambao hawajui nia Zangu ni wale wasiojua jinsi ya kutafuta, na wataachwa, wataondolewa! Ni dhahiri kwamba, kugundua nia Zangu ni somo la kwanza ambalo lazima mjifunze. Ni kazi ya dharura zaidi, na hairuhusu kuchelewa! Msisubiri Mimi nimkaripie kila mmoja wenu, mmoja baada ya mwingine! Ninyi daima ni wasiojali na wapumbavu. Ni jambo la mzaha! Siwezi kuamini ninyi ni wapumbavu hivi! Hamjali kuhusu nia Zangu! Jiulizeni, ni mara ngapi ninyi huelewa nia Zangu kabla ya kutenda? Mnapaswa kuwa ndio mnaojifunza wenyewe! Mnataka Niwashughulikie mmoja mmoja, hiyo haiwezekani! Mnapaswa kujifunza kupata uzoefu na kupata utambuzi na hekima mnapotenda. Maneno yanayotoka vinywani mwenu ni mazuri, lakini hali halisi ni ipi? Mnapokumbana na uhalisi hamtaweza kufanya chochote. Mnachosema hakilingani na uhalisi. Kwa kweli Siwezi kuvumilia kile ambacho ninyi mnafanya; Natazama na Siwezi kujizuia kuwa na huzuni. Kumbukeni hili! Katika siku zijazo jifunzeni kutambua nia Zangu!

Sura ya 55

Ule unaodaiwa kuwa ubinadamu wa kawaida si wa kimwujiza sana kama watu wanavyofikiria, lakini unaweza kuvuka mipaka ya pingu za watu wote, matukio, na vitu, na mateso yatokanayo na mazingira ya mtu. Unaweza kunikaribia Mimi na kuwasiliana kwa karibu na Mimi mahali popote au katika hali yoyote. Ninyi daima hutafsiri vibaya nia Zangu. Ninaposema mnapaswa kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida, mnajizuia na kudhibiti miili yenu. Lakini huzingatii kutafuta kwa makini ndani ya roho, ila kwa kile mnachovaa kwa nje pekee, ukikosa kuangalia ufunuo Wangu ndani yako, na kulisimua Kwangu ndani yako. Jinsi ulivyo mzembe! Mzembe sana! Inaweza kuwa kwamba kumaliza kile ambacho Nimekuaminia ni ufanisi mkubwa? Wewe ni mpumbavu! Huzingatii kukita mizizi kwa kina! “Usiwe jani kwa mti, ila uwe mzizi wa mti huo”—huo kweli ni wito wako? Hujali! Mzembe! Unaridhika punde unapofikiria kuwa umepata mapato kidogo. Jinsi unavyojali mapenzi Yangu kidogo sana! Kuanzia sasa, sikiliza, usiwe baridi na usiwe hasi! Unapohudumu, Nikaribie mara kwa mara na kuwasiliana kwa karibu na Mimi. Hii ndiyo njia yako ya pekee. Najua kwamba tayari umejinyima, unajua upungufu wako mwenyewe, unajua udhaifu wako mwenyewe. Lakini kujua tu hakutoshi. Unahitaji kushirikiana na Mimi na punde unapoelewa nia Zangu ziweke katika vitendo mara moja. Hii ndiyo njia bora kabisa ya kuonyesha kujali mzigo Wangu, njia bora kabisa ya kutii.

Bila kujali jinsi unavyonitendea, Nataka kutekeleza mapenzi Yangu kwako na watakatifu wote, na Nataka mapenzi Yangu yatekelezwe bila kuzuiwa katika nchi yote. Tambua hili kikamilifu! Hili linahusu amri Zangu za utawala! Huogopi hata kidogo? Hutetemeki kwa hofu kwa sababu ya vitendo vyako na mienendo yako? Miongoni mwa watakatifu wote karibu wote hawahisi nia Yangu. Hutaki kuwa wa kipekee kama mtu anayefikiria mapenzi Yangu kabisa? Je, wajua? Nia yangu ya dharura kwa sasa ni kutafuta kundi la watu wanaoweza kufikiria mapenzi Yangu kabisa. Hutaki kuwa mmoja wao? Hutaki kujitumia kwa ajili Yangu, kujitolea kwa ajili Yangu? Hutaki kulipa gharama hata kidogo, kutoa juhudi hata kidogo! Mambo yakiendelea kuwa hivyo, juhudi Yangu ya bidii itakuwa bure kwenu. Baada ya Mimi kukuonyesha hilo, bado hujaelewa uzito wa suala hili?

“Kwa wale wanaotumia rasilimali kwa dhati kwa ajili Yangu, hakika Nitakubariki sana.” Unaona! Nimekuambia hili mara kadhaa, lakini bado una mashaka mengi, ukiogopa mazingira ya jamii, ukiogopa mazingira ya nje. Kweli hujui kinachokufaa! Nawatumia tu watu waaminifu, wa kawaida, na wazi. Umekuwa na furaha na radhi kwa Mimi kukutumia, lakini kwa nini bado una wasiwasi sana? Inaweza kuwa kwamba maneno Yangu hayana athari hata kidogo kwako? Nimesema kuwa Nakutumia wewe, ilhali huwezi kuamini hilo kwa uthabiti. Kila mara unashuku, ukiogopa kwamba Nitakuacha. Dhana zako zimefungwa sana! Ninaposema kwamba Nakutumia hilo linamaanisha Nakutumia. Kwa nini una shaka sana kila mara? Je, ni kwamba Sijaongea kwa wazi vya kutosha? Kila neno ambalo Nimesema ni kweli. Hakuna tamko hata moja ambalo si la kweli. Mwanangu! Niamini. Jitolee nafsi kwa niaba Yangu, na hakika Nitajitolea nafsi kwako!

Sura ya 56

Nimeanza kuchukua hatua kuadhibu wale ambao hufanya uovu, wale ambao hushika madaraka, na wale ambao hutesa wana wa Mungu. Kuanzia sasa kuendelea, mkono wa amri Zangu za utawala utakuwa daima juu ya wale wanaonipinga mioyoni mwao. Fahamu hili! Huu ndio mwanzo wa hukumu Yangu, na hakuna huruma itakayoonyeshwa kwa yeyote wala hakuna atakayesamehewa, kwani Mimi ni Mungu asiyependelea ambaye hutenda haki, na ingekuwa vyema kwenu nyote kutambua hili.

Si kwamba Nataka kuadhibu wale ambao hufanya uovu, badala yake ni adhabu inayoletwa kwao na uovu wao wenyewe. Mimi siwi na haraka ya kumwadhibu yeyote, wala Simtendei yeyote bila haki—Natenda haki kwa wote. Kwa hakika Napenda wana Wangu na hakika Nachukia wale waovu wasionitii; hii ndiyo kanuni ya matendo Yangu. Kila mmoja wenu anapaswa kuwa na umaizi wa amri Zangu za utawala. Iwapo sivyo, hamtakuwa na hofu hata kidogo na mtakuwa wazembe mbele Yangu, na hamtajua kile Ninachotaka kutimilisha, kile

Ninachotaka kufanya kuwa kamili, kile Ninachotaka kupata ama ufalme Wangu unahitaji mtu wa aina gani.

Amri Zangu za utawala ni:

1. Haijalishi wewe ni nani, ukinipinga Mimi katika moyo wako, utahukumiwa.
2. Kwa wale ambao Nimechagua, watafundishwa nidhamu mara moja kwa sababu ya wazo lolote lisilo sahihi.
3. Nitawaweka wale wasioniamini kwa upande mmoja. Nitawaruhusu wazungumze na kutenda kwa uzembe hadi mwisho kabisa ambapo Nitawaadhibu kabisa na kupambana nao.
4. Kwa wale ambao wananiamini, Nitawatunza na kuwalinda nyakati zote. Nyakati zote Nitawapa uzima kwa kutumia njia ya wokovu. Watu hawa watakuwa na upendo Wangu na hakika hawataanguka ama kupoteza njia yao. Udhaifu wowote ambao wako nao utakuwa wa muda, na kwa hakika Sitaukumbuka.
5. Kwa wale ambao wanaonekana kuamini lakini ambao kwa kweli hawaamini—kumaanisha wale ambao wanaamini kuna Mungu lakini hawamtafuti Kristo, lakini ambao pia hawapingi—watu wa aina hizi ni wa kusikitisha zaidi, na kupitia vitendo Vyangu Nitawafanya waone kwa dhahiri. Kupitia matendo Yangu, Nitawaokoa watu wa aina hizi na kuwarudisha.
6. Wazaliwa wa kwanza ambao walikuwa wa kwanza kukubali jina Langu watabarikiwa! Hakika Nitawapa baraka bora zaidi na mtakuwa na furaha hadi kuridhika kwa mioyo yenu; hakuna atakayethubutu kuizuia. Kila kitu kimetayarishwa kabisa kwa ajili yenu, kwani hii ni amri Yangu ya utawala.

Katika vipengele vyote, mnapaswa kuweza kuona kile mkono Wangu hufanya na fikira ambazo Ninazo katika moyo Wangu—yote si kwa ajili Yenu? Ni nani kati yenu aliye upande Wangu? Je, mmechunguza fikira katika mioyo yenu ama maneno ambayo ninyi husema? Je, mmekaribia kwa uangalifu sana mambo haya? Wapumbavu! Wapotovu! Kutokubali vizuizi vya Roho Mtakatifu! Nimekuwa nikiiachilia sauti Yangu tena na tena ndani yako, lakini hakujakuwa na mjibizo wowote hata kidogo. Usiwe mpumbavu tena! Wajibu wako ni kuelewa mapenzi Yangu; aidha, ni njia unayopaswa kuingia. Umekanganyikiwa, huna umaizi, huoni kwa dhahiri kile Ninachotaka kutimiza ndani Yako, ama kile Ninachotaka kupata kutoka kwako! Ili kuelewa mapenzi Yangu lazima kwanza uanze kwa kunikaribia na kushiriki zaidi na Mimi. Daima unasema kwamba huwezi kuelewa mapenzi Yangu; tayari umejazwa na mambo yako mwenyewe, basi Naweza kufanya kazi kwako? Huji mbele Yangu kwa vitendo, lakini unasubiri tu kwa uhasi. Nasema wewe ni kama mnyoo, ilhali unahisi kukosewa na hulikubali.

Wakati huu unapaswa kuinuka na kushirikiana na Mimi! Usiwe hasi! Hiyo itarudisha maisha yako nyuma. Kuwa wa vitendo huleta manufaa kwako, sio kwa wengine—bado hujatambua na kuelewa hili? Mapenzi yangu daima hufichuliwa kwako—hujayatambua? Mbona hujawahi kuyatilia maanani? Na mbona hujawahi kuweza kuelewa mapenzi Yangu? Je, kushika mapenzi Yangu hakukuletei manufaa?

Natumai unaweza kufikiria mapenzi Yangu kwa hali zote ili Niweze kuwa na njia ya kuendea na maskani ya kupumzikia ndani yako. Usinizuie tena, ni ukatili sana! Huna uelewa wa maneno Yangu na huyatolei hisia. Tazama na uone wakati ni upi sasa—hakuwezi kuwa na kusubiri zaidi! Usipofuata nyayo Zangu kwa ukaribu basi muda utakuwa umeisha, sembuse kuwepo njia yoyote ya wewe kuukomboa!

Sura ya 57

Je, umechunguza kila fikira na mawazo yako, na kila tendo lako? Uko wazi kuhusu gani kati ya haya yanalingana na mapenzi Yangu na gani hayalingani? Huna uwezo wa kutambua haya! Mbona hujaja mbele Yangu? Je, ni kwa sababu Sitakuambia, au ni kwa ajili ya sababu nyingine? Unapaswa kujua hili! Kujua kwamba wale walio wazembe hawawezi kuyaelewa mapenzi Yangu kabisa au kupokea mwangaza na ufunuo mkuu.

Je, umegundua sababu kanisa haliwezi kupata lishe na linakosa ushirika wa kweli? Unajua ni vipengele vigapi ambavyo vimesababisha haya vinahusiana na wewe? Nilikuagiza kutoa uhai na kuachilia sauti Yangu. Umefanya haya? Unaweza kuwajibikia kuchelewesha maendeleo ya ndugu zako katika maisha? Unapokabiliwa na masuala umekuwa mwenye wasiwasi badala ya kuwa mtulivu na makini. Kweli wewe ni mjinga! Sauti Yangu inapaswa kuachiliwa kwa watakatifu. Usizuie kazi ya Roho Mtakatifu na usinicheleweshee muda; hakuna kati ya hayo inayofaidi yeyote. Nataka ujitolee kikamilifu kwa ajili Yangu, kimwili na kiakili, ili kwamba kila wazo na fikira yako iwe kwa ajili Yangu, ili uweze kushiriki mawazo Yangu na wasiwasi Wangu, na kwamba kila kitu unachofanya kitakuwa kwa ajili ya ufalme wa leo na usimamizi Wangu, na si kwa ajili yako. Hilo pekee ndilo litaunidhisha moyo Wangu.

Chochote ambacho Nimefanya hakikosi ithibati. Mbona hujaniiga? Mbona hujatafuta ithibati kwa ajili ya kile unachofanya? Unataka Niseme nini zaidi? Nilikuchukua kwa mkono kukufundisha, lakini umeshindwa kujifunza—wewe ni mjinga sana! Unataka kuanza tena? Usivunjike moyo. Ni lazima ujikaze tena na kujitoa kikamilifu kwa niaba ya matumaini yaliyoshirikiwa na matakwa yaliyoshirikiwa ya watakatifu. Kumbuka maneno hayo: “Kwa wale wanaotumia rasilmali kwa dhati kwa ajili Yangu, hakika Nitakubariki sana.”

Chochote unachofanya lazima ukifanye kwa mpango, sio ovyoovy. Kweli unathubutu

kusema unajua hali ya watakatifu kama unavyojua kiganja cha mkono wako mwenyewe? Hilo linaonyesha unakosa hekima, kwamba hujachukulia suala hili kwa uzito hata kidogo, na hujatumia muda wowote kwalo. Ikiwa kweli ungeweza kutumia muda wako wote kwa hilo, ona vile hali yako ya ndani ingekuwa. Hatafuti kutoa juhudi za nafsi ila unatafuta tu sababu zisizopendelea na huonyeshi fikira hata kidogo kwa mapenzi Yangu—hilo limenihuzunisha sana! Usiendeleo hivi! Inaweza kuwa kwamba hukubali baraka ambazo Nimekupa?

Ee, Mungu! Mwana Wako ni mdeni Wako. Sijachukulia kazi Yako kwa uzito, au kufikiria mapenzi Yako, wala sijakuwa mwaminifu kwa ushawishi Wako. Mwana Wako anataka kugeuza haya yote. Naomba Usiniache, na naomba Uendeleo kutekeleza kazi yako kunipitia. Ee, Mungu! Usimwache mwana Wako yeye peke yake, ila andamana nami kila wakati. Ee, Mungu! Mwana Wako anajua Unanipenda, lakini siwezi kuyaelewa mapenzi Yako, sijui jinsi ya kufikiria mzigo Wako, na sijui jinsi ya kutimiza kile ambacho Umeniaminia, sembuse kujua jinsi ya kuliongoza kanisa. Unajua kwamba mimi ni mwenye huzuni na majonzi juu ya hili. Ee, Mungu! Tafadhali Niongoze nyakati zote. Ni sasa tu ninapohisi jinsi ninavyokosa, nahisi vyema sana! Siwezi kulieleza kabisa. Acha mkono Wako wenye enzi uonyeshe neema kwa mwana Wako, msaidie mwana Wako nyakati zote, na mfanye mwana Wako aweze kujihusudu kabisa mbele Yako, asifanye uamuzi wake tena, asiwe na fikira na mawazo yake tena. Ee, Mungu! Unajua kwamba mwana Wako anataka kufanya kila kitu kwa ajili Yako kabisa, kwa ajili ya ufalme leo kabisa. Unajua ninachofikiri na ninachofanya wakati huu. Ee, Mungu! Nichunguze Wewe mwenyewe. Naomba tu kwamba Utembee nami na kubaki nami katika maisha haya nyakati zote, ili nguvu Yako iandamane na matendo yangu.

Sura ya 58

Ukielewa nia Yangu, utaweza kuufikiria mzigo Wangu na unaweza kupata mwanga na ufunuo, na kupata ufunguliwaji na uhuru, kuuridhisha moyo Wangu, kuyaruhusu mapenzi Yangu kwa ajili yako kutekelezwa, kuwaletea watakatifu wote ujenzi wa maadili, na kuufanya ufalme Wangu duniani kuwa imara na thabiti. Jambo la muhimu sasa ni kuelewa nia Yangu, hii ni njia mnayopaswa kuingia katika na hata zaidi ni wajibu wa kutimizwa na kila mtu.

Neno Langu ni dawa nzuri inayoponya kila aina ya maradhi. Alimradi uko tayari kuja mbele Yangu, Nitakuponya, na kukuruhusu kuona kuwepo kwa kudura Yangu, kuona matendo Yangu ya ajabu, kuona haki na uadhama Wangu na hata zaidi kuona upotovu wenu wenyewe na udhaifu wenu wenyewe. Naelewa kabisa kila hali ndani yako; daima unafanya vitu ndani ya moyo wako na hauonyeshi kwa nje. Niko wazi hata zaidi kuhusu kila kitu unachokifanya. Lakini unapaswa kujua ni vitu gani Ninavyovisifu, na ni vitu gani Nisivyovisifu; unapaswa kutofautisha kwa wazi hivi viwili na haupaswi kuchukulia hili kwa kawaida.

Unaunga mkono kwa maneno matupu tu, ukisema “Lazima tufikirie mzigo wa Mungu.” Lakini unapokabili ukweli, huufikiri vya kutosha ingawa unajua vizuri mzigo wa Mungu ni nini. Kweli umevurugwa kabisa, mjinga kwa kiwango fulani, na hata zaidi mshenzi kikamilifu. Hili linaeleza jinsi mwanadamu alivyo mgumu kushughulikia na yote anayofanya ni kuunga mkono kwa maneno matupu yanayosikika kuwa mazuri, akisema kitu kama “Siwezi kabisa kuielewa nia ya Mungu, lakini nikielewa hakika ninatenda kulingana nayo.” Hii si hali yenu ya kweli? Ingawa nyote mnajua nia ya Mungu, na mnajua chanzo cha ugonjwa wenu ni kipi, jambo la muhimu ni kwamba hamko tayari kutenda; huu ni ugumu mkubwa zaidi. Usipotatua hili mara moja, litakuwa kikwazo kikubwa zaidi kwa maisha yako mwenyewe.

Sura ya 59

Tafuta mapenzi Yangu zaidi katika mazingira unayoyakabili na kwa hakika utapata kibali Changu. Alimradi uwe tayari kwenda katika utafutaji na kuhifadhi moyo ambao unanicha, Mimi Nitakupea yote unayokosa. Kanisa sasa linaingia utendaji rasmi na mambo yote yanaingia kwenye alama sahihi. Mambo hayako yalivyokuwa wakati ilikuwa limbuko la mambo yajayo; lazima msiwe wa kuchanganyikiwa au mkose utambuzi. Ni kwa nini Mimi nahitaji kwamba muingie ndani ya uhalisi katika kila kitu? Je, kweli umelipitia jambo hili? Je, mnaweza kweli kunikidhi Mimi katika kile Ninachohitaji kwenu, kama vile Ninavyowakidhi nyinyi? Usiwe mdanganyifu! Sio zaidi ya stahamala Yangu kwenu tena na tena na bado hamna uwezo wa kujua ni kipi kizuri kwenu tena na tena, na kukosa kuonyesha shukrani!

Haki Yangu, uadhama Wangu, hukumu Yangu, na upendo Wangu—mambo yote haya Ninayomiliki, mambo Niliyo—je, umeyaonja hayo kwa kweli? Kweli nyinyi ni wapumbavu sana na hamtambui mapenzi Yangu. Nimewaambia tena na tena kwamba ninyi wenyewe lazima muonje karamu Ninazozindaa, lakini mnazitupa tena na tena na hamuwezi kutofautisha mazingira mazuri na yale mbaya. Ni gani kati ya mazingira haya yamebuniwa na nyinyi wenyewe? Na ni gani ambayo yamepangwa kwa mikono Yangu? Msijitete! Ninaona kila kitu kwa dhahiri kabisa na ni tu kwamba usitafute. Nini zaidi Ninaweza sema?

Daima Nitawaridhisha ambao wanatambua mapenzi Yangu na Mimi sitawaruhusu wateseke au wapate madhara. Jambo la muhimu sasa ni kwamba mna uwezo wa kuchukua hatua kwa mujibu wa mapenzi Yangu, na wale ambao wanatenda hili kwa hakika watapokea baraka Zangu na kuwa chini ya ulinzi Wangu. Ni nani kati yenu kwa kweli anaweza kabisa kutumia rasilimali kwa ajili Yangu na kutoa yote yao kwa ajili Yangu? Nyinyi nyote mu shingo upande, mawazo yenu yanaenda pande zote, yakifikiria juu ya nyumbani, dunia ya nje, chakula na mavazi. Licha ya ukweli kwamba uko mbele Yangu ukifanya mambo kwa ajili Yangu, katika moyo wako bado unafikiria mke, watoto na wazazi wako walio nyumbani. Je, haya yote ni mali yako? Mbona

usiwakabidhi mikononi Mwangu? Je, hunisadiki vya kutosha? Au ni kwamba unahofia Nitafanya mipango isiyofaa juu yako? Mbona daima wewe huwa na wasiwasi kuhusu familia yako ya mwili? Wewe huwatamani sana wapendwa wako! Je, Ninamiliki nafasi fulani moyoni mwako? Na bado unazungumzia kuhusu kuniruhusu Mimi kutawala ndani yako na kumiliki nafsi yako nzima—haya yote ni uongo mdanganyifu! Ni wangapi kati yenu ambao ni wa kanisa kwa mioyo yenu yote? Na ni nani kati yenu hawafikiri juu yao, lakini ni wa ufalme wa leo? Fikiria kwa makini sana kuhusu hili.

Mmenisukuma hadi kiasi hiki, hivyo Ninaweza kutumia tu mikono Yangu kuwachochea mbele; Sitawashawishi tena mbele. Hii ni kwa sababu mimi ni Mungu Mwenye hekima, na Mimi huwatendea watu tofauti kwa njia tofauti, kutegemea jinsi ninyi ni waaminifu Kwangu. Mimi ni Mungu Mwenyezi—ni nani anathubutu kuzuia hatua Zangu za mbele? Yeyote anayethubutu kuniasi, mkono wa amri Zangu za utawala kuanzia sasa kuendelea utakuwa milele juu yao, ili kwamba wapate kujua uweza Wangu. Kile Ninachotaka si idadi kubwa ya watu, lakini ufanisi. Mimi Nitamuacha na kumwadhibu yeyote ambaye ni muasi, mdanganyifu, yeyote anayejiughulisha katika tabia potovu na ya ulaghai. Usifikirie tena kuwa Mimi ni Mwenye rehema, au kwamba Mimi ni mwenye upendo na mkarimu; huku ni wewe kujifurahisha tu. Najua kuwa Nitakavyokuendelea zaidi ndivyo zaidi unaendelea kuwa hasi na kutoonyesha hisia zaidi, na hutakuwa tayari kujitoa mwenyewe. Wakati watu ni wagumu kwa kiasi hiki Ninaweza tu kuwachochea wao na kuwalazimisha wao mbele wakati wote. Fahamu hili! Kuanzia sasa Mimi ni Mungu Ambaye Anahukumu; Mimi tena si mwenye rehema, mkarimu na mwenye upendo tena wa ubunifu wa mtu!

Sura ya 60

Si jambo rahisi kwa maisha kukua; yanahitaji mchakato, na aidha, kwamba muweze kulipa gharama na kwamba mshirikiane na Mimi kwa uwiano, na hivyo mtapata sifa Yangu. Mbingu na dunia na vitu vyote vinaanzishwa na kufanywa kamili kupitia maneno Nitamkayo, na chochote kinaweza kutimizwa nami. Matakwa Yangu ya pekee ni kwamba mkue haraka, mchukue mzigo kutoka kwa mabega Yangu na kuuweka kama wenu, mfanye kazi Zangu kwa niaba Yangu, na hilo litauridhisha moyo Wangu. Ni mwana yupi angekataa mizigo ya babake? Ni baba yupi hangefanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya mwana wake? Lakini ninyi hamwelewi mapenzi Yangu, hamfikirii mizigo Yangu, maneno Yangu hayana maana kwenu na hamfanyi jinsi maneno Yangu yanavyosema. Daima mnajitawala; ninyi ni wabinafsi kiasi gani! Mnajifikiria wenyewe tu!

Je, kwa kweli unaelewa mapenzi Yangu, au unajifanya kutoelewa? Kwa nini daima unajishughulisha na mienendo mitundu kama hiyo? Je, dhamiri yako inasema kuwa unanitendea

haki kwa kufanya hivyo? Ukishapata chanzo cha ugonjwa, mbona huwasiliani na Mimi ili upate matibabu? Nitakuambia: Kuanzia siku hii kuendelea hamtakuwa na magonjwa ya mwili tena. Sehemu yenu yoyote ikihisi gonjwa msijishughulisha kutafuta chanzo cha nje. Badala yake, kujeni mbele Yangu na kutafuta kujua nia Yangu—mtakumbuka hili? Hii ni ahadi Yangu: Kuanzia siku hii kuendelea mbele mtaondoka kwa mwili wenu kabisa na kuingia dunia ya roho, yaani, mwili wenu hautasumbuliwa na ugonjwa tena. Mnafurahia hilo? Mnahisi furaha? Hii ni ahadi Yangu na aidha, kile ambacho mmetamani kwa muda mrefu. Leo kimetimika kwa ninyi mliobarikiwa; jambo la ajabu na lisiloeleweka vipi!

Kazi Yangu inaendelea usiku na mchana; muda kwa muda, haikomi kamwe. Hii ni kwa sababu tamaa Yangu ya dharura ni kukufanya uupendeze moyo Wangu, na kwamba moyo Wangu utafarijiwa na ninyi hivi karibuni. Wana Wangu! Wakati umefika wa ninyi kushiriki katika baraka Zangu za wema! Zamani, ninyi mliteseka kwa ajili ya jina Langu, lakini sasa siku zenu za majaribu zimekwisha. Yeyote akijaribu kuumiza unywele kutoka kwa vichwa vya Wanangu, Sitamsamehe kwa urahisi, wala wao hawataweza kuinuka tena. Hii ni amri Yangu ya utawala na yeyote atakayekiuka hii atajihatarisha. Wanangu! Furahieni mpaka mridhike! Imbeni na kuita kwa shangwe! Hamtadhulumiwa na kukandamizwa tena, na hamtapitia mateso tena. Hamtalazimika kuwa waoga juu ya imani yenu Kwangu; mnapaswa kutangaza hadharani imani yenu Liiteni jina Langu takatifu kwa sauti ya kutosha kufanya ulimwengu na miisho ya dunia kutingika. Acha wao waone, wale waliowaangalia kwa dharau, walioangamizwa na kuteswa na wao, leo kuwa na mamlaka juu yao na kuwatawala, waongoze, na, muhimu zaidi, wahukumu.

Mnapaswa kujihusisha na kuingia kwenu pekee, na Nitawapa baraka hata nzuri zaidi ili mweze kuzifurahia, na baraka hizi zitawaruhusu kuonja utamu wao usiolinganika vyema zaidi na kuhisi kwa nguvu siri zao zisizoisha na kwamba ni kubwa sana kuelewa!

Sura ya 61

Ukiwa na ufahamu wa hali yako mwenyewe basi utafanikisha mapenzi Yangu. Kwa kweli, mapenzi Yangu si magumu kushika, ni kwamba tu katika siku zilizopita hukuweza kutafuta kulingana na lengo Langu. Ninachotaka si dhana wala fikira za binadamu, sembuse pesa zako wala mali yako. Ninachotaka ni moyo wako, unaelewa? Haya ni mapenzi Yangu, na hata zaidi ni kitu ambacho Nataka kupata. Watu daima hutumia dhana zilizo akilini mwao kunifanyia maamuzi, na kuhakiki kimo Changu wakitumia Vipimo vyao. Kwa binadamu, hiki ni kitu kigumu sana kujihusisha nacho, na ndicho Ninachokichukia na kusinywa nacho zaidi, mnaona? Kwa sababu hii ndiyo tabia ya Shetani inayoonekana zaidi. Na vimo vyenu ni vidogo, hivyo kila mara mnaanguka katika njama za kijanja za Shetani. Hamuwezi hata kuzitambua! Nimewaambia mara nyingi muwe waangalifu kila wakati na kwa kila namna, kwamba msidanganywe na

Shetani. Lakini hamskilizi na kwa wepesi wa moyo mnapuuza Ninayoyasema, hivyo mnaishia kupoteza maishani mwenu na majuto huja yakiwa yamechelewa mno. Vyovyote vile, si itakuwa vizuri kwako kuchukua hili kama funzo kwa ajili ya kutafuta kwako kwa baadaye. Nakwambia, kuwa hasi kwa urahisi kutaleta hasara kwa maisha yako na itakuwa yenye ukali mwingi zaidi. Kwa kujua hili, unafaa uamke, sivyo?

Watu wana pupa ya matokeo ya haraka na wanaona tu yalio mbele ya macho yao. Ninaposema Nimeanza kuwaadhibu walio mamlakani, mnakuwa hata wenye wasiwasi zaidi, na mnauliza: “Mbona watu hao bado wako mamlakani? Si Mungu amezungumza maneno matupu?” Dhana za binadamu zimekita mizizi sana! Hamwelewi maana ya yale Nisemayo. Wale ambao Nawaadhibu ni wale waovu, wale ambao wananidharau, wale ambao hawanifahamu, na Nawapuuza wale wanaoniamini lakini hawatafuti ukweli. Nyinyi ni wapumbavu sana! Hamjaelewa yale ambayo Nimesema hata kidogo! Ingawa hii ndiyo hali, bado mnajisifu mkifikiri kwamba mmekomaa, kuwa mnaelewa mambo na kuwa mnaweza kufahamu mapenzi Yangu. Mara kwa mara Mimi husema vitu vyote na mambo yote yanamtumikia Kristo, lakini kwa kweli mnayaelewa maneno haya? Mnayajua maneno haya kweli? Nimesema awali kuwa Simwadhibu mtu yeyote bila subira. Kila mtu katika ulimwengu dunia hufuata mipango Yangu inayofaa: Wale ambao ni walengwa wa adhabu Yangu, wale wanaomtumikia Kristo (hawa Sitawaokoa), wale ambao wameteuliwa na Mimi, na wale ambao wamechaguliwa nami lakini baadaye wanakuwa walengwa wa kuondolewa, wote hawa Ninawashika mkononi Mwangu, bila hata kukutaja wewe—ambaye Nimemchagua—ambaye Ninamwelewa hata zaidi. Vitu Nifanyavyo katika awamu hii na vitu Nitakavyovifanya katika awamu ijayo vyote vinafuata mipango Yangu ya busara. Huhitaji kupanga lolote kwa ajili Yangu kabla; ngoja tu starehe yako! Hiki ni kitu ambacho unastahili. Natawala vitu vilivyo Vyangu na Sitawahurumia kwa wepesi wale watakaothubutu kunung’unika ama watakaothubutu kuwa na maoni mengine kunihusu. Mara kwa mara siku hizi Ninalipuka kwa hasira, kwa kuwa mpango wa amri za utawala ambazo Nimepanga zimeendelea hadi katika hatua hii. Usifikiri kuwa Sina hisia. Kwa kuwa Nimesema awali hakuna mtu hata mmoja, tukio ama kitu kinachothubutu kuzuia hatua Zangu za kuendelea. Natenda Nisemayo, na hiki ndicho Mimi nilicho, na hata zaidi ni dalili inayoonekana sana ya tabia Yangu. Nawatendea watu wote kwa usawa, kwani nyote ni wana Wangu, na Nawapenda nyote. Ni baba yupi asiyechukua wajibu wa maisha ya mwanawe? Ni baba yupi hafanyi bidii usiku na mchana kwa ajili ya siku za baadaye za mwanawe? Na nani kati yenu anaweza kujua? Nani anaweza kuuonyesha moyo Wangu huruma? Daima mnapanga mipango na utaratibu wa anasa zenu za kimwili na hamna utambuzi wowote wa moyo Wangu. Ninauhangaisha moyo Wangu hadi unavunjika kwa sababu yenu, lakini daima mnazitamani anasa za kimwili, kula na kunywa, kulala, jinsi mnavyovaa—hamna dhamiri hata kidogo? Kama hii ndiyo hali, basi ninyi

ni wanyama waliovalia nguo za binadamu. Ninayosema si yasiyostahili na lazima muweze kuyastahimili. Hii ndiyo njia nzuri kabisa ya kuwaokoa na hata zaidi ni pahali ambapo hekima Yangu ipo—kuupiga udhaifu wa nguvu za Shetani, kumshinda kabisa na kumwangamiza kabisa. Mradi tu mtubu na kuhakikisha kuwa mnaweza kuntegemea Mimi kuindoa asili ya zamani na kuishi kwa kudhihirisha umbo la mtu mpya, moyo Wangu utaridhika kikamilifu, kwani huku ni kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida, kuwa na ushuhuda kwa jina Langu, na ndicho kinachonifurahisa zaidi.

Kila wakati lazima uwe karibu na Mimi, na inaweza kuonekana kuwa mwendo Wangu unaongeza kasi siku kwa siku. Kama wakati wowote unakosa ushirika wa kiroho, basi hukumu Yangu italetwa juu yako mara moja. Kwa hoja hii una ufafanuzi wa kina. Sio kwa sababu Sikupendi ndiyo Nakuadibu, bali Nakufunza nidhamu kwa sababu ya upendo Wangu kwako. Vinginevyo hungekua na daima ungepotoshwa bila kuzuiwa na Roho Mtakatifu. Hii hata zaidi ni uso wa hekima Yangu.

Sura ya 62

Kuyaelewa mapenzi Yangu hakufanywi ili tu kwamba uweze kujua, ila pia kwamba uweze kutenda kulingana na nia Yangu. Watu hawauielewi moyo Wangu. Ninaposema huku ni mashariki, wanalazimika kuenda na kutafakari, wakijiuliza, “Kweli ni mashariki? Pengine sio. Siwezi kuamini kwa urahisi hivyo. Nahitaji kujionea mwenyewe.” Ninyi watu ni wagumu sana kushughulikia, na hamjui utii wa kweli ni nini. Mnapojua nia Yangu kisha mwende kuitenda kwa kusita—hakuna haja ya kuifikiria! Daima unashuku Ninachokisema na kukielewa kwa upuuji, hivyo basi unawezaje kuwa na utambuzi wowote wa kweli? Kamwe hutafuti kuingia katika maneno Yangu. Kama ambavyo Nimesema awali, Ninachotamani ni wachache waliochaguliwa, sio watu wengi sana. Wale wasioweka umuhimu kwa kuingia katika maneno Yangu hawastahili kuwa askari wazuri wa Kristo, ila badala yake wanatenda kama vikaragosi vya Shetani na kuingilia kazi Yangu. Usifikiri hili ni suala dogo. Yeyote anayeingilia kazi Yangu anazikosea amri Zangu za utawala, na bila shaka Nitamfundisha nidhamu kwa ukali. Yaani, kuanzia sasa kuendelea, ukigeuka kutoka Kwangu kwa muda basi hukumu Yangu itakufikia. Usipoyaamini maneno Yangu basi jaribu ujionee, uone ni hali gani uliyo katika ukiishi katika mwanga wa uso Wangu, na uko katika hali gani unaponiacha.

Siogopi kwamba huishi katika roho. Kazi Yangu imeendelea hadi kwa hatua ya sasa, hivyo unaweza kufanya nini? Nafanya vitu kwa hatua, hivyo hakuna haja ya wewe kuwa na wasiwasi. Nitafanya kazi Yangu Mimi mwenyewe. Ninapofanya kitu watu wote wanaridhishwa kabisa, vinginevyo Nitawashughulikia kwa kuwadibu kwa ukali zaidi. Hili linahusisha amri Zangu za utawala zaidi. Inaweza kuonekana kwamba amri Zangu za utawala tayari zimeanza sasa

kutangazwa na kutekelezwa, zisifichwe tena. Ni lazima uone hili kwa uwazi! Sasa heshima zote zinahusu amri Zangu za utawala na yeyote anayezikosea lazima apate hasara. Hili bila shaka si suala dogo. Kweli mnatambua hili? Mnaelewa kipengele hiki vizuri kabisa? Sasa Naanza kushiriki: Mataifa yote na watu wote wa dunia wanaongozwa mikononi Mwangu na, bila kujali dini yao, wote lazima waje kwa kiti Changu cha enzi. Bila shaka, wengine wanaopokea hukumu watatupwa katika shimo la kina kirefu (ni walengwa wa uangamizi ambao watateketezwa kabisa na hawatabaki tena), na wengine wanaokubali jina Langu baada ya kuhukumiwa watageuka watu wa ufalme Wangu (watafurahia kwa miaka 1,000 pekee). Wale kati yenu watakaoshikilia ufalme na Mimi milele baadaye, na kwa vile awali mliteseka kwa ajili Yangu, Nitabadilisha mateso yenu na baraka Nitakazowapa bila kikomo; wale kati ya watu Wangu watabaki tu wakitoa huduma kwa Kristo. Hiyo raha hairejelei tu raha, ila badala yake kwamba wale watu wanawekwa mbali na kupitia maafa. Hii ndiyo maana ya ndani ya matakwa Yangu kwenu sasa kuwa makali zaidi, na kuhusu kila kitu sasa kugusa amri Zangu za utawala. Kwa maana iwapo hamkukubali mafundisho Yangu basi hakungekuwa na njia ya Mimi kuwapa kile mnachopaswa kurithi. Ingawa hali iko hivi, bado mnaogopa kuteseka, mnaogopa majeraha yafikie roho zenu, daima mkifikiri kuhusu mwili na daima mkipanga na kuratibu kwa ajili yenu wenyewe. Je, Sijawafanyia mipango ya kuwafaa ninyi? Hivyo kwa nini tena na tena unajifanyia mipango yako mwenyewe? Unanitukana! Sivyo? Ninakupangia kitu lakini unakikana kabisa na kufanya mipango yako mwenyewe.

Mnaweza kuzungumza vyema, lakini kwa hakika hamtii mapenzi Yangu hata kidogo. Nakuambia, Sitasema kabisa kwamba kuna yeyote miongoni mwenu ambaye anaweza kuyafikiria mapenzi Yangu kwa kweli. Ingawa vitendo vyako vinaweza kukubaliana na mapenzi Yangu Sitakusifu hata kidogo. Hii ni njia Yangu ya wokovu. Ingawa hali iko hivi, bado mnaridhika wakati mwingine, mkijiona kuwa wa kushangaza na kuwadharau wengine wote. Hiki ni kipengele kimoja cha tabia potovu ya mwanadamu. Nyote mnakubali hoja hii Ninayotoa, lakini juu juu pekee. Ili kuweza kubadilika kwa kweli unahitaji kunikaribia; kushiriki na Mimi na Nitakupa neema. Watu wengine wanafikiri kukaa kwa kutulia tu na kuvuna kile ambacho wengine wamekipanda, wakihihi kwamba ili kuvaa mavazi, wanahitaji tu kunyoosha mikono yao, na ili kula, wanahitaji tu kufungua midomo yao, hata wakingojea wengine wawatafunie chakula chao kabla wawe radhi kukimeza. Watu kama wao ni wapumbavu zaidi, wanaopenda kula kile ambacho wengine wamekila tayari, na hili ni dhihirisho la kipengele kizembe zaidi cha mwanadamu. Kwa kusikia haya maneno Yangu, ni lazima usiyapuuze tena. Kutahadhari kabisa ndio njia sahihi pekee. Kisha mapenzi Yangu yanaweza kuridhishwa, na huu ni utii wa aina bora zaidi.

Sura ya 63

Zielewe hali zako mwenyewe, na zaidi ya hayo, kuwa wazi kuhusu njia unayohitaji kutembea; usubiri tena Mimi niyainue masikio yako na kukuonyesha mambo. Mimi ni Mungu ninayeangalia moyo wa ndani kabisa wa mwanadamu nami najua kila fikra na wazo lako, hata zaidi Naelewa matendo na tabia yako. Lakini matendo yako na tabia yana ahadi Yangu? Je, yana mapenzi Yangu? Umetafuta haya kwa kweli? Je, kweli umetumia wakati wowote kuhusu suala hili? Je, kweli umefanya jitihada yoyote? Mimi sikukosoi. Ninyi mnapuza tu kipengele hiki! Siku zote mmechanganyikiwa na hamwezi kuona chochote kwa uwazi. Je, mnaifahamu sababu ya hili ni nini? Je, ni kwa sababu mawazo yenu hayako wazi na dhana zenu zina msingi madhubuti sana, na kuongeza kwamba ukweli kwamba hamuonyeshi fikira zozote kuhusu mapenzi Yangu. Baadhi ya watu watasema: “Unawezaje kusema hatuonyeshi fikira zozote kuhusu mapenzi Yako? Mara kwa mara tunajaribu kuelewa mapenzi Yako, lakini hatuwezi kuyaelewa, hivyo tunaweza kufanya nini? Je, kweli Unaweza kusema kwamba sisi hatufanyi jitihada yoyote?” Acha nikuulize: Je, unathubutu kusema kwamba kweli wewe ni mwaminifu Kwangu? Na nani anathubutu kusema kwamba anajitoa Kwangu katika uaminifu kamili? Nina hofu kwamba hakuna mmoja kati yenu anayeweza kusema hivi. Kwa sababu, ni wazi Mimi kusema, kila mmoja wenu ana uwezo wake wa kuchagua na mambo yake mwenyewe anayoyapenda, na hata zaidi nia zenu wenyewe. Msiwe wadanganyifu! Nilielewa kabisa zamani sana yote mnayoyafikiria mioyoni mwenu; bado Nahitaji kufafanua hili? Lazima uchunguze zaidi kutoka katika kila kipengele (mawazo na dhana zako, kila kitu unachosema, kila neno, kila nia na motisha katika kila hatua unayoichukua); kwa njia hii utapata kufikia kuingia kila kipengele, na hata zaidi utakuwa na uwezo wa kujiandaa na ukweli kamili.

Kama Singewaambia hivi bado mngekuwa mmechanganyikiwa, mkitamani anasa za mwili kwa siku nzima, bila ya hamu yoyote ya kuonyesha mapenzi Yangu nadhari yoyote. Daima Nautumia mkono Wangu wenye upendo kuwaokoa, mnajua hivyo? Je, mmekuja kutambua hili? Nakupenda kwa dhati; unathubutu kusema unanipenda kwa dhati? Jiulize, unaweza kweli kuja mbele zangu kupokea ukaguzi Wangu kuhusu kila tendo lako? Je, unaweza kweli kuniruhusu Nichunguze kila mwenendo wako? Nasema umepotoka nawe uko tayari kujitetea. Hukumu Yangu inakujia; sasa lazima uamke katika ukweli! Yote Nisemayo ni ukweli, na yanaonyesha hali halisi ndani yako. Aa, wanadamu! Ninyi ni wagumu sana kuwashughulikia. Ni wakati tu Ninapokuonyesha hali yako halisi ndipo mnaamini katika mioyo na kwa neno. Nisipofanya hivi, basi kila mara mnashikilia mawazo yenu ya zamani na kushikamana na njia zenu za kufikiri, mkifikiri kwamba hakuna mtu yeyote duniani aliye mwerevu zaidi yenu. Je, hivi si wewe ni mwenye kujidai? Je, si ni wewe kujiingiza katika majisifu na kuridhika, na majivuno? Sasa unapaswa kutambua hili! Usijidhani mwerevu au wa ajabu, lakini badala yake ni lazima uwe

daima na ufahamu wa mapungufu yako mwenyewe na tabia zako mwenyewe yenye udhaifu. Kwa njia hii, azimio lako la kunipenda halitapungua, lakini litakuwa imara zaidi na zaidi, na hali zako mwenyewe zitakuwa bora na bora zaidi; muhimu zaidi maisha yako yataendelea zaidi milele, siku baada ya siku.

Utakapofahamu mapenzi Yangu basi utajijua, na hivyo kunijua Mimi bora zaidi na kuendelea zaidi katika uhakika wako kunihusu Mimi. Katika wakati wa sasa, kama mtu hawezi kufikia asilimia tisini wa uhakika kunihusu Mimi, lakini badala yake anaendelea kuwa juu dakika moja na chini dakika ya pili, akiwa moto na baridi, basi Nasema mtu huyo kwa hakika ni kitu cha kuachwa. Asilimia kumi iliyobaki hutegemea kabisa nuru na mwangaza Wangu, hivyo kufikia asilimia mia moja ya uhakika kunihusu. Sasa hivi, kumaanisha leo, wangapi wanaweza kupata aina hii ya kimo? Daima Nayaonyesha mapenzi yangu kwako na hisia za maisha daima zinakimbia ndani yako, hivyo kwa nini usitende kulingana na Roho? Je, una hofu ya kufanya makosa? Hivyo basi kwa nini usizingatie mazoezi kabisa? Nakwambia, huwezi kufahamu mapenzi Yangu kwa kujaribu mara moja au mbili; lazima kuwe na mchakato. Nimesema hivi mara nyingi, hivyo kwa nini usiiweke katika vitendo? Je, hufikiri unakuwa mkaidi? Unataka kumaliza kila kitu mara moja, huko radhi kamwe kufanya juhudi yoyote au kutumia muda wowote kwa kitu chochote. U mpumbavu jinsi gani na hata zaidi u mjinga!

Je, hamfahamu kwamba daima Mimi huzungumzia mambo bila kuyaficha maneno Yangu? Kwa nini daima ninyi ni wapumbavu, wenye kutojali na wagumu kuelewa? Mnapaswa kujichunguza zaidi, na mnapaswa kuja mbele Zangu mara nyingi zaidi ikiwa kunacho kitu chochote msichOkielewa. Nasema kwako, Nazungumza kwa njia hizi mbalimbali ili kuwaelekeza mbele Zangu; kwa nini, baada ya muda mrefu sana, bado hamtambui hili? Je, ni kwa sababu maneno Yangu yamewafanya nyote kuchanganyikiwa? Au ni kuwa bado hamjashughulikia kila moja ya maneno Yangu kwa uzito? Mnapoona maneno Yangu mnakuwa na ufahamu mzuri kujihusu wenyewe, na mnasema kuwa mnanidai au kwamba hamuwezi kuyafahamu mapenzi Yangu. Na baada ya hayo? Ni kama hamjakuwa na lolote la kufanya na vitu hivi, kana kwamba wewe si mtu tu ambaye anaamini katika Mungu. Je, si wewe tu unapokea tu habari kwa haraka bila kujipa muda wa kuiwaza? Wakati unayafurahia maneno Yangu, ni kama kutazama maua kwa haraka ukiwa kwenye mgongo wa farasi, bila kujaribu kamwe kufahamu mapenzi Yangu ndani ya maneno Yangu. Hivi ndivyo watu walivyo: Mara zote wao hupenda kuonekana wanyenyekevu, na aina hii ya mtu ni mwenye kuchukiza zaidi. Wanapokuwa pamoja na wengine kushiriki, siku zote hupenda kusambaza ufahamu wao kujihusu mbele ya watu wengine, na kuwafanya wengine waone kwamba wao ni mtu ambaye anaonyesha kuufikiria mzigo Wangu, wakati kwa kweli wao ni wajinga zaidi. (Hawashiriki umaizi wao ama ufahamu wao kweli kunihusu Mimi na ndugu zao, lakini badala yake wanajiweka wenyewe tu katika maonyesho na

kujionyesha mbele ya watu wengine, Nawachukia watu hawa kabisa, kwa kuwa wao hunikashifu na kuniumbua.)

Mara kwa mara Mimi huifanya wazi miujiza yangu mikubwa zaidi kwenu—hamuwezi kuiona? Kile kinachoitwa ukweli kinaishi kwa kudhihirishwa na wale ambao wananipenda kwa dhati—hamjaiona? Si hili ni thibitisho bora ambalo mnaweza kunijua? Je, hili halishuhudii bora Kwangu? Lakini hamlitambui hilo. Niambieni, nani anaweza kuishi kwa kudhihirisha hali halisi katika dunia hii iliyochangamana ambayo ni chafu, yenye taka, na iliyopotoshwa na Shetani? Si watu wote ni waovu na watupu? Hata hivyo, maneno Yangu yamefikia kilele chake; hakuna maneno ambayo yanaweza kueleweka kwa urahisi zaidi kuliko haya. Hata mpumbavu mkubwa anaweza kuyasoma maneno Yangu na kuyaelewa, hivyo si kwamba ninyi tu hamjafanya jitihada yoyote?

Sura ya 64

Unapaswa kutoelewa maneno Yangu kwa njia ya upuuzi; unapaswa kuelewa maneno Yangu kwa kuangalia vipengele vyote na unapaswa kujaribu kuyaelewa zaidi na kuyafikiri sana kwa kurudia, sio tu kwa siku moja ama usiku mmoja. Hujui mahali ambapo mapenzi Yangu yapo ama ni katika kipengele kipi Nalipa gharama Yangu ya bidii za kazi; unawezaje kuyazingatia mapenzi Yangu? Ninyi watu mko hivi; hamna uwezo wa kuchunguza kwa utondoti, mkisisitiza tu sehemu ya juu na mkiwa tu na uwezo wa uigaji. Hii inawezaje kuitwa mambo ya roho? Ni shauku ya mwanadamu tu, ni kile ambacho Sikisifu na zaidi ni kile ambacho Nakichukia sana. Nakwambia, vitu vyote ambavyo Navichukia sana lazima viondolewe, lazima vidhoofike katika maafa, na lazima vipitie uhomaji Wangu na hukumu Yangu. Vinginevyo watu hawatajua “hofu” inamaanisha nini na watakuwa wamepotoshwa sana, daima wakiniona na macho ya mwanadamu—ni wapumbavu sana! Kuja karibu na Mimi na kufanya ushirika na Mimi ni njia bora zaidi ya kuondoa mawazo ya Shetani. Nataka ninyi nyote mtende kulingana na amri hii kuepuka kuhukumiwa na kupatwa na hasara katika maisha yenu.

Mwanadamu ni mgumu sana kushughulikia, daima akiwa chini ya udhibiti wa watu wa nje, matukio, na mambo na chini ya udhibiti wa dhana zake mwenyewe, hivi kwamba hawawezi kuwa na ushuhuda mzuri kwa ajili Yangu na hawana uwezo wa kushirikiana vyema na Mimi. Mimi daima huwasaidia na kuwakimu, ilhali hamwezi tu kufanya kila mnaloweza kushirikiana na Mimi. Hivi vitu vyote vinaonyesha kwa kutosha ukosefu wenu wa ufahamu Kwangu. Wakati utakapofika ambapo huna tena shaka zozote kabisa kunihusu, basi hakuna mtu anayeweza kukuzuia kutembelea njia ya kweli, na hakuna dhana za mwanadamu zinaweza kukuzuia. Mbona Nasema hili? Kweli unaelewa maana ya maneno Yangu? Ni wakati tu ambapo Nabainisha maneno kama haya ndipo mna ufahamu mdogo. Watu ni wajinga hivi na ni dhaifu sana

kichwani. Ni wakati tu ambapo sindano inagonga mfupa ndipo wanaanza kuhisi uchungu kidogo. Yaani, wakati tu ambapo maneno Yangu yanaonyesha chanzo cha ugonjwa wako ndipo unashawishika kabisa. Hata kama hali iko hivi, wakati mwingine bado hamtaki kuweka maneno Yangu katika vitendo, na hamtaki kujijua. Sasa, mbona bado hamjatambua jinsi mwanadamu ni mgumu kushughulikia? Je, ni kwamba maneno Yangu hayazungumzwi dhahiri ama wazi kikamilifu? Ninachotaka ni ninyi kushirikiana na Mimi kwa bidii na kwa dhati; bila kujali iwapo unazungumza maneno yanayosikika kuwa ya kufurahisha au la, mradi uko radhi kushirikiana na Mimi na unaweza kuniabudu na moyo wako wa kweli, basi utakuja chini ya ulinzi Wangu. Hata kama mtu wa aina hii ni mpumbavu sana Nitampa nuru ili aweze kutoa upumbavu wake. Hii ni kwa sababu matendo Yangu lazima yakubaliane na kile Ninachosema; Mimi ni Mwenyezi Mungu ambaye kamwe hatoi ahadi ambayo Hawezi kutimiza.

Mapenzi Yangu yatafichuliwa mara moja kwa makanisa yote na wazaliwa wa kwanza wa kiume wote, hakuna kitakachofichwa tena asilani, kwani siku ambayo yote yanafichuliwa imewadia. Hiyo ni kusema kwamba neno “fichwa” kuanzia sasa halitatumiwa, sembuse chochote ambacho kimefichwa kuwepo. Watu, matukio na mambo yote ambayo yamefichwa lazima yafunuliwe moja moja. Mimi ni Mungu wa busara Anayeshika mamlaka tele. Matukio yote, mambo yote na kila mtu, yote yako katika mikono Yangu. Nachukua hatua Zangu mwenyewe kuyafunua na Nitayafunua yote moja baada ya nyingine, kwa njia ya mtindo mzuri. Kwa yeyote anayethubutu kunirairai au kujaribu kuficha chochote kutoka Kwangu, Nitahakikisha hatainuka tena. Nitachukua hatua kwa njia hii ili nyote muweze kuona hilo. Tazama kwa udhahiri! Gharama ya bidii za kazi ambayo Nimelipa si bure lakini itazaa matunda. Yeyote asiyetilia maanani ama kutii atapambana na hukumu Yangu mara moja. Ni nani ambaye bado anathubutu kuenda dhidi Yangu? Ni lazima nyote mnitii. Nasema kwako, kila kitu Ninachosema na kufanya, kila tendo, kila wazo, fikira na mpango Ninayo leo ni sahihi, na hayamwachii mwanadamu nafasi ya kufikiria. Mbona Ninawaambia tena na tena kwamba mnahitaji tu kufuata na hakuna haja ya kulifikiria tena? Ni kwa sababu hii; bado mnahitaji Nilibainishe?

Dhana zenu zinawazuia, lakini hamfikiri kwamba ni kwa sababu ninyi wenyewe hamjajitahidi, badala yake mkinitazama kwa ajili ya sababu, mkisema kwamba Sijakupa nuru—haya ni mazungumzo ya aina gani? Hamwajibiki wenyewe, daima mkinilalamikia. Ninakuonya! Ukiendelea hivi, kutolipa gharama yoyote, basi utatupwa! Sijidai siku nzima ili kuwatisha. Huu kwa kweli ni ukweli, na Mimi hufanya kile Ninachosema. Punde tu maneno yanapotoka kinywani Mwangu, mara moja yanaanza kutimizwa. Kabla, maneno Niliyoyazungumza yalitimizwa polepole. Lakini sasa mambo ni tofauti, na mambo hayatafanyika polepole tena. Kwa kusema waziwazi, Sishawishi na kubembebeza tena, lakini badala yake Nawahimiza na kuwalazimisha, Kulisema hata wazi zaidi, wale wanaoweza kuenda kwa mwendo sawa hufanya

hivyo; wale wasioweza kuenda kwa mwendo sawa na hawawezi kuendelea kutembea wataondolewa. Zamani, Niliwazungumzia kwa subira kwa kila njia, lakini hasa hamkusikiza. Kwa kuwa sasa kazi imeendelea hadi hatua hii, mtafanya nini? Bado mnajifurahisha? Mtu wa aina hii hawezi kufanywa kuwa mkamilifu, lakini hakika atakuwa chombo cha kuondolewa na Mimi!

Sura ya 65

Maneno Yangu daima yanaendeleza barabara, yaani yanaonyesha udhaifu wenu wa jaala, vinginevyo bado mngekuwa mnakokota visigino vyenu, bila wazo la muda gani ulioko sasa. Fahamu hili! Mimi Hutumia njia ya upendo ili kuwaokoa. Bila kujali jinsi nyinyi mlivyo, bila shaka Nitakamilisha mambo ambayo Nimekubali bila kufanya kosa lolote. Je, Ninaweza, Mwenyezi Mungu Mwenye haki, kufanya kosa? Je, hiyo siyo dhana ya mtu? Niambieni, kila kitu Mimi Hufanya na kusema si kwa ajili yenu? Baadhi ya watu kwa unyenyekevu watasema: “Ee Mungu! Unafanya kila kitu kwa ajili yetu, lakini hatujui jinsi ya kushirikiana na Wewe.” Upumbavu ulioje! Kusema kwamba hamjui jinsi ya kushirikiana na Mimi! Yote hayo ni uongo za aibu! Kwa kuwa mnasema mambo kama haya, kwa nini, katika hali halisi, mara kwa mara mnaonyesha fikira kwa mwili? Maneno yenu ni matamu, lakini hamtendi kwa njia ya furaha na ya kupendeza. Lazima muelewa hili: Kile ambacho Ninahitaji leo kutoka kwenu sio kuomba mengi, wala hakiko nje ya ufahamu wenu, lakini kinaweza kutimizwa na mtu. Siwakadiri kupita kiasi; je, Mimi sijui ukubwa wa uwezo wa mtu? Ninauelewa kwa uwazi kamili.

Maneno Yangu huwapa nuru daima, lakini mioyo yenu yamefanywa kuwa ngumu mno na hamuwezi kuelewa mapenzi Yangu ndani ya roho zenu! Niambieni, ni mara ngapi Nimewakumbusha msisisitiza juu ya chakula, mavazi na kuonekana kwenu, lakini badala yake kusesitiza maisha ya ndani? Lakini nyinyi hamsikilizi. Nimechoka kuisema. Je, mmekuwa ambao hamjali kiasi hiki? Je, mmekuwa wapumbavu kabisa? Je, ingewezekana kuwa maneno Yangu yamenenwa bure? Je, Nimesema lolote ambalo si sahihi? Wanangu! Muwe na busara kwa nia Zangu zenye ari! Wakati maisha yenu yamekomaa, hakutakuwa na haja ya kuwa na wasiwasi, na kila kitu kitatolewa. Hakuna thamani katika kusesitiza mambo hayo kwa sasa. Ufalme Wangu umefanikishwa kabisa na umekuja chini katika dunia kwa umma; hata zaidi hii inamaanisha kuwa hukumu Yangu imetokea kabisa. Je, mmeipitia? Mimi Ninachukia kabisa kuwahukumu nyinyi, lakini hamuonyeshi moyo Wangu fikira hata kidogo. Napenda kwa hicho ambacho mnapata mara kwa mara kuwa utunzaji na ulinzi wa upendo Wangu, na wala sio hukumu ya kikatili. Je, ingewezekana kuwa mko tayari kuhukumiwa? Kama si hivyo, mbona basi mara kwa mara hampati kuwa karibu nami, kushiriki na kuwasiliana na Mimi? Nyinyi hunichukulia Mimi kwa ubaridi sana, na wakati Shetani anakupa mawazo unahisi kufurahishwa, ukifikiri kwamba

yanapatana na mapenzi yenu wenyewe, lakini hakuna kitu mnachofanya ni kwa ajili Yangu. Je, mnataka siku zote mnichukulie kwa ukatili?

Siyo kwamba Mimi sitaki kukupatia wewe, lakini kwa kuwa hamko tayari kulipa gharama, basi mko mikono mitupu, bila kushika chochote kabisa. Je, hamuoni kwamba kazi ya Roho Mtakatifu sasa inaendelezwa kwa haraka sana? Je, hamwoni kwamba moyo Wangu unakosa subira sana? Ninawaomba mshirikiane na Mimi lakini mnabaki kutotaka. Maafa yote yatatokea moja baada ya nyingine; mataifa yote na maeneo yote yatapitia maafa—tauni, njaa, mafuriko, ukame na matetemeko ya ardhi yatakuwa kila mahali. Maafa haya hayatokei tu sehemu moja au mbili, wala hayataisha kwa siku moja au mbili, lakini badala yake yataeneza juu ya eneo kubwa zaidi na zaidi, na maafa yatakuwa makali zaidi na zaidi. Wakati huu kila namna ya wadudu tauni watatokea kwa mfululizo, na tukio la watu kuwala watu litatokea kila mahali. Hii ni hukumu Yangu juu ya mataifa yote na watu. Wanangu! Lazima msipate maumivu wala shida za maafa. Napenda hivi karibuni nyinyi mkomae na mchukue mzigo ulioko kwenye mabega Yangu haraka iwezekanavyo; kwa nini nyinyi hamelewi mapenzi Yangu? Kazi iliyo mbele itahitaji juhudi nyingi zaidi na zaidi. Je, mu wenye moyo mgumu hadi kuniacha Mimi na mikono Yangu iliyojaa, kufanya kazi kwa bidii sana Pekee Yangu? Nitanena wazi zaidi; Wale ambao maisha yao hukomaa wataingia katika hifadhi na hawatateseka maumivu au taabu; wale ambao maisha yao hayakomai lazima wateseke maumivu na madhara. Maneno Yangu ni dhahiri ya kutosha, sivyo?

Jina Langu lazima litandazwe katika pande zote na kila mahali, kwamba kila mtu alijue jina Langu takatifu na kunijua Mimi. Watu wa kutoka kila pembe za dunia Marekani, Japani, Kanada, Singapore, Umoja wa Kisovyeti, Macau, Hong Kong na nchi nyingine watasongamana mara moja katika Uchina kwa pamoja, wakitafuta njia ya kweli. Jina Langu tayari limeshawashuhudia wao; kila kilichobaki ni nyinyi mkomae mapema iwezekanavyo ili mpate kuchunga na kuwaongoza. Hii ndiyo maana Nasema kwamba kuna hata kazi zaidi inayopasa kufanywa. Jina Langu litaenea nje katika mwamko wa maafa, na msipochunga mtapoteza sehemu inayopaswa kuwa yenu; je, hamuogopi? Jina Langu huenea kwa dini zote, na kila pembe za dunia, mataifa yote na madhehebu yote. Hii ni kazi Yangu inayofanywa kwa utaratibu, katika viungo vinavyohusiana kwa karibu, yote hutendeka kwa mipango Yangu ya busara. Ningependa tu muwe na uwezo wa kuendelea mbele kwa kila hatua, kwa karibu mkifuata nyayo Zangu.

Sura ya 66

Kazi Yangu imeendelea hadi hatua ya sasa na yote imefuata mipango ya busara ya mkono Wangu, na pia kuwa fanikio Langu kuu. Nani kati ya wanadamu anaweza kufanya kitu kama hiki? Na je, si wanaona ni afadhali waingilie kati usimamizi Wangu? Lakini lazima ujue kuwa

hakuna namna yeyote anaweza kufanya kazi Yangu badala Yangu, sembuse kuizuia, kwani hakuna yeyote anayeweza kusema au kufanya vitu Nifanyavyo na kusema. Ingawa hii ndio hali, watu bado hawanijui Mimi—Mwenyezi Mungu mwenye busara! Huthubutu kunikataa kwa wazi, ilhali unajiweka dhidi Yangu katika mioyo yenu na kwa akili zenu. Wapumbavu! Je hujui Mimi ni Mungu ambaye Anatazama moyo wa ndani kabisa wa mwanadamu? Je hujui kwamba Naangalia kila neno na tendo lako? Nasema kwako, Sitawahi tena kutamka maneno ya upole kutoka kwa midomo Yangu. Badala yake yote yatakuwa maneno ya hukumu kali, na Nitaona kama unaweza kuyastahimili au la. Kutoka sasa kuendelea, wale ambao mioyo yao haiko karibu na Mimi, ikimaanisha wale ambao hawana upendo wa dhati Kwangu, ndio wale ambao wananikataa Mimi kwa wazi.

Leo, kazi ya Roho Mtakatifu imefika katika hatua ambapo mbinu ya awali haihitaji kutumika tena, lakini badala yake mbinu mpya sasa inaingiwa. Wale ambao hawashirikiani na Mimi vyema na kikamilifu wataanguka Kuzimu, lindi kuu ya kifo (watu hawa watapitia maangamizi milele). Mbinu mpya ni kama ifuatavyo: Kama moyo wako na akili haviko sawa basi hukumu Yangu itakuangukia mara moja, na hii inajumuisha kushikilia dunia, mali, familia, mume, mke, watoto, wazazi, kula na kunywa na nguo na vitu vyote vilivyo nje ya ulimwengu wa kiroho. Kupata nuru kwa watakatifu kutaonekana zaidi, yaani, hisia za maisha zitakuwa dhahiri zaidi na zitakuwa zikisonga kila mara. Yeyote anayesababisha pingamizi hata kidogo atapata kuanguka kuliko na maafu na ataanguka nyuma zaidi katika njia ya mbio za maisha. Wale ambao ni vuguvugu, ambao hawatafuti kwa kujitolea Nawaacha kabisa na kuwapuuzwa wote bila kumwacha yeyote, na watadhoofika kwa majanga kwa miaka elfu. Wale wanaotafuta kwa shauku, yaani, wale ambao wanadakiza kila wakati, Nitatupa ujinga wao na kuwafanya kuwa waaminifu Kwangu, na zaidi watakuwa na busara na akili, na hivyo watatafuta kwa imani kuu hata zaidi. Naweka baraka Zangu maradufu juu ya wana Wangu wazaliwa wa kwanza na upendo Wangu unakuja juu yenu kila wakati. Nawaangalia na kuwalinda kila wakati na Sitakubali muanguke katika mtego wa Shetani. Nimeanza kuzindua kazi Yangu kati ya watu wote; yaani, Nimeongeza mradi mwingine wa kazi. Hao ni wao ambao watatoa huduma kwa Kristo kwa miaka elfu, na idadi kubwa mno ya watu itasongamana katika ufalme Wangu.

Wana Wangu, lazima mzidishe mazoezi yenu. Kuna kiwango kikubwa cha kazi kinachowangoja, kazi ambayo lazima ufanye na kumaliza. Nataka tu uharakishe na ukomae, ili kumaliza kazi ambayo Nimekukabidhi. Hili ni jukumu lako takatifu, na ni wajibu ambao lazima ufanywe na wale kati yenu ambao ni wana Wangu wazaliwa wa kwanza. Nitawalinda hadi mwisho wa njia na kuwalinda ili muweze kufurahia furaha kamili na Mimi milele! Kila mmoja wenu lazima awe na ufahamu katika ukweli kuwa Nimepanga dhabihu nyingi na kupanga mazingira mengi, yote ili kuwakamilisha ninyi. Mnajua kuwa zote hizi ni baraka Zangu, sivyo?

Ninyi nyote ni wana Wangu wapendwa. Mradi tu mnanipenda Mimi kwa dhati basi Sitamwacha hata mmoja wenu, ingawa hili linategemea kama mnaweza kushirikiana kwa upatanifu na Mimi au la.

Sura ya 67

Wana Wangu wanaonekana wazi, na wanaonekana mbele ya watu wote. Nitawaadhibu vikali wale wanaothubutu kuwakataa wao kwa wazi; hiyo ni hakika. Leo, wale wote wanaoweza kusimama na kuchunga kanisa sasa wamepata cheo cha mzaliwa wa kwanza na sasa wako pamoja katika utukufu Na Mimi—yale yote yaliyo Yangu ni yenu pia. Ninawakabidhi wale wanaonitii Mimi kwa dhati neema tele, ili uweze kuwa wenye nguvu, zaidi ya nguvu ya wanadamu wengine. Mapenzi Yangu yako juu yenu kwa ukamilifu wana wazaliwa wa kwanza na Nawatakia tu mkomae haraka iwezekanavyo na mkamilishe yale ambayo Nimewapa. Jua hili! Yale ambayo Nimewapa ni mradi wa mwisho wa mpango Wangu wa usimamizi. Ninatarajia tu muweze kunipa Mimi nafsi yako yote kwa moyo wako wote, akili yako yote na nguvu yako yote, na utumie rasilimali kwa ajili Yangu. Muda kweli haumngoji mtu yeyote, na hakuna yeyote, au suala, na hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kuzuia kazi Yangu. Jua hili! Kazi Yangu inaendelea taratibu bila kizuizi katika kila hatua.

Nyayo Zangu zinatembea katika ulimwengu wote na katika miisho ya dunia, macho Yangu yanachunguza kila mtu daima, na hata zaidi Natazama picha yote ya ulimwengu. Maneno Yangu ya utendaji yanafika katika kila pembe ya ulimwengu. Yeyote anayethubutu kutotoa huduma yake Kwangu, yeyote anayethubutu kutokuwa mwaminifu Kwangu, yeyote anayethubutu kulihukumu jina Langu, na yeyote anayethubutu kuwatukana na kuwapaka tope wana Wangu—wale wote ambao kwa kweli wanafanya vitu hivi lazima wapitie hukumu kali. Hukumu Yangu inaanguka kikamilifu. Hivi ni kusema, sasa ni enzi ya hukumu, na kwa uchunguzi wa makini utapata kuwa hukumu Yangu inaendelea kote katika ulimwengu dunia. Bila shaka, familia Yangu haijaachwa; wale ambao fikira zao, maneno, na vitendo havipatani na mapenzi Yangu watahukumiwa. Lazima uelewe, hukumu Yangu inaelekezwa kwa ulimwengu dunia wote, sio tu kikundi kimoja cha watu ama vitu—je, umegundua hili? Ikiwa unapambana kimawazo kunihusu kwa dhati, basi utahukumiwa ndani yako mara moja.

Hukumu Yangu huja kwa maumbo na aina zote. Jua hili! Mimi ni Mungu wa kipekee na wa busara wa ulimwengu dunia! Hakuna kitu kinachozidi nguvu Yangu. Hukumu Zangu zote zimefichuliwa kwako: Ikiwa unapambana kimawazo kunihusu, Nitakutia nuru kama onyo. Kama hutasikia, basi Nitakuacha mara moja (hili halihusu kushuku jina Langu, lakini kwa tabia za nje—zile zinazohusu raha za kimwili). Kama mawazo yako ni ya kunikataa, unanilalamikia, unakubali tena na tena mawazo ya Shetani na hufuati hisia za maisha, basi roho yako itakuwa

gizani na mwili wako utapitia uchungu. Lazima uwe karibu na Mimi. Hutaweza kabisa kurejesha hali yako ya kawaida kwa siku moja au mbili tu, na maisha yako yataonekana kubaki nyuma zaidi. Wale ambao hotuba yao haifai Nitaadhibu midomo yako na ndimi na kufanya ndimi zako kupitia ushughulikaji. Wale ambao bila kupinga ni wapotovu kwa matendo Nitakuonya kwa roho zenu, na Nitaadhibu vikali wale ambao hawasikii. Wale ambao wananihukumu na kunikana kwa wazi, yaani wale ambao wanaonyesha kutotii kwa neno ama kwa tendo, Nitawaondoa kabisa na kuwaacha, Nitawafanya kuangamia na kupoteza baraka za juu; hao ni wale ambao wanaondolewa baada ya kuchaguliwa. Wale ambao ni wajinga, yaani wale ambao maono yao sio wazi, bado Nitawapa nuru na kuwaokoa. Lakini wale ambao wanaelewa ukweli lakini hawauweki katika vitendo watapewa adhabu kulingana na sheria ambazo zimetajwa awali, iwe hawajui au la. Kwa wale watu ambao nia zao hazijakuwa sahihi tangu mwanzo, Nitawafanya wasiweze milele kuelewa uhalisi na mwishowe wataondolewa hatua kwa hatua, mmoja kwa mmoja—hakuna hata mmoja atakayebaki—lakini wanabaki sasa kwa mpango Wangu (kwani Sifanyi vitu kwa haraka, ila kwa mtindo wa utaratibu).

Hukumu Yangu imefichuliwa kabisa, imelengwa kwa watu tofauti, na wote lazima wachukue nafasi zao zinazostahili. Ikitegemea ni sheria gani iliyovunjwa, Nitawaadhibu na kuwahukumu kulingana na sheria hiyo. Na kwa wale ambao hawako katika jina hili na hawamkubali Kristo wa siku za Mwisho, kuna sheria moja tu: Nitachukua roho mara moja, roho na mwili wa yeyote anayenikataa na kuwatupa Kuzimu; wowote ambao hawanikatai Mimi, Nitangoja mkomae kabla ya kufanya hukumu ya pili. Maneno Yangu yanaeleza yote kwa uwazi kamili na hakuna kilichofichwa. Ninatarajia tu kuwa mtaweza kuyaweka akilini kila wakati!

Sura ya 68

Neno Langu linatekelezwa katika kila nchi, mahali, taifa na kikundi, na neno Langu linakamilishwa katika kila pembe wakati wowote. Maafa yanayotokea kila mahali si vita kati ya watu, wala si mapigano na silaha. Hakutakuwa na vita tena baadaye. Wote wako katika mfumbato Wangu. Wote watakabili hukumu Yangu na watadhoofika kati ya maafa. Acha wale wanaonipinga na wale wasioanza kushirikiana na Mimi wateseke uchungu wa maafa mbalimbali. Acha walie na kusaga meno yao hadi milele, na kubaki katika giza daima. Hawataendelea kuishi. Natenda kwa unyoofu na wepesi, na Sifikiri jinsi umekuwa mwaminifu Kwangu zamani. Alimradi unipinga, mkono Wangu wa hukumu utakuachia huru ghadhabu kwa haraka bila kuchelewa hata kidogo, si hata sekunde, na bila chembe ya huruma. Nimekuwa Nikisema wakati huu wote kwamba Mimi ni Mungu anayetimiza neno Lake. Kila neno Ninalolisema litakamilishwa, na mtaona yote. Hii kweli ndiyo maana ya kuingia katika uhalisi katika kila kitu.

Maafa makuu hakika hayatawafikia wana Wangu, wependwa Wangu. Nitawatunza wana

Wangu kila wakati na kila sekunde. Hakika hamtavumilia uchungu na mateso hayo; badala yake, ni kwa ajili ya ukamilishwaji wa wana Wangu na utimizaji wa neno Langu ndani yao, ili kwamba muweze kutambua kudura Yangu, mkue zaidi katika maisha, mbebe mizigo kwa ajili Yangu karibuni, na kujitolea kabisa kwa ukamilisho wa mpango Wangu wa usimamizi. Mnapaswa kuwa na furaha na kuridhika na kushangilia kwa sababu ya hili. Nitawapa kila kitu, Nikiwaruhusu kuchukua usukani. Nitaiweka mikononi mwenu. Mwana akirithi mali nzima ya babake, je, ninyi wana Wangu wazaliwa wa kwanza mtaridhi zaidi kiasi gani? Kweli mmebarikiwa. Badala ya kuteseka kutokana na maafa makuu, mtafurahia baraka za milele. Utukufu ulioje! Utukufu ulioje!

Ongeza kasi yako, na ufuate nyayo Zangu kila mahali na nyakati zote; usibaki nyuma. Acheni mioyo yenu iufuate moyo Wangu, na akili zenu ziifuate akili Yangu. Shirikiani na Mimi kwa moyo mmoja, akili moja. Kuleni nami, ishi nami, na kufurahia nami. Baraka za ajabu zinawasubiri kufurahia na kuchukua. Kuna utele mwingi usiolinganishika ndani Yangu. Hakuna hata kidogo kimetayarishwa kwa ajili ya mtu mwingine—Nafanya hili kwa ajili ya wana Wangu kabisa.

Sasa, Nilicho nacho akilini ndicho kitakachotimizwa. Punde ambapo Nimemaliza kuwasemea, masuala hayo tayari yamekamilishwa. Kazi kweli inaendelea haraka hivyo na inabadilika wakati wowote. Uangalifu wako ukipotea hata kwa muda, tukio la “kani nje” litatokea, na utatupwa mbali sana, na utaondoka kutoka kwa mkondo huu. Iwapo hamtafuti kwa ari mtaacha juhudi Zangu za uangalifu kuwa bure. Baadaye, watu kutoka mataifa mbalimbali watakusanyika wakati wowote. Katika kiwango chenu cha sasa, mtaweza kuwaongoza? Nitawafunza kikamilifu kuwa askari wazuri katika kipindi hiki kidogo cha muda ili kukamilisha agizo Langu. Ningependa mlitukuze jina Langu katika kila hali na kuwa na ushuhuda wa ajabu kwa ajili Yangu. Acha wale waliowadharau wakue juu yao leo na kuwaongoza na pia kuwatawala. Je, mnaelewa nia Zangu? Mmetambua juhudi Zangu za uangalifu? Nafanya haya yote kwa ajili yenu. Inategemea iwapo mnaweza kufurahia baraka Zangu au la.

Mimi, Mungu anayechunguza akili na moyo wa mwanadamu, Nasafiri kwa miisho ya dunia. Nani anayethubutu kutofanya huduma kwa ajili Yangu? Migogoro inaongezeka miongoni mwa mataifa yote na wanapambana kwa ukali, lakini hatimaye hawataepa kutoka kwa mfumbato Wangu. Hakika Sitawaruhusu waponyoke kwa urahisi. Nitawaleta kwa hukumu mmoja mmoja kwa msingi wa matendo yao, hadhi za kidunia, na raha za dunia. Sitamsamehe yeyote. Hasira Yangu imeanza kufichuliwa na yote itawajia. Yote yatatimizwa ndani yao mmoja mmoja na hiki kitakuwa kile walichojiletea wao wenyewe kabisa. Wale waliokosa kunijua au walionidharau zamani sasa watakabili hukumu Yangu. Na kuhusu wale waliowatesa wana Wangu zamani, hasa

Nitawaadibu kwa mujibu wa kile walichokisema na kukifanya. Sitawaacha hata watoto. Wote ni wa namna ya Shetani. Hata wasiposema na kufanya chochote, kama wanawachukia wana Wangu mioyoni mwao, Sitamwacha hata mmoja wao. Nitawafanya wote waone kwamba wale wanaotawala na kushikilia mamlaka leo ni sisi, kundi hili la watu, hakika sio wao. Kwa sababu hii, nyote mnapaswa kutoa nguvu yenu ya juu sana na kwa kweli mjitumie kwa ajili Yangu, ili kulitukuza na kulishuhudia jina Langu katika kila mahali, pembe, dini na dhehebu, na mlienze katika ulimwengu mzima na miisho ya dunia!

Sura ya 69

Mapenzi Yangu yatokapo, yeyote anayethubutu kupinga na yeyote anayethubutu kuhukumu au kuwa na shaka, mara moja Nitamfukuza. Leo, yeyote ambaye hatendi kulingana na mapenzi Yangu, au yeyote anayeyafikiria mapenzi Yangu visivyo, ni lazima atupwe nje na kuondolewa kutoka kwa ufalme Wangu. Katika ufalme Wangu hakuna mtu mwingine—wote ni wana Wangu wa kiume, wale ambao Nawapenda na hunifikiria Mimi. Zaidi ya hayo, ndio ambao hutenda kulingana na neno Langu na ambao wana uwezo wa kutawala katika uongozi kwa niaba Yangu kuhukumu mataifa yote na watu wote. Aidha, wao ni kundi la wana wa kiume wazaliwa wa kwanza, ambao ni maasumu na wa kuisimua; sahili na wazi; waaminifu na wenye hekima. Mapenzi Yangu yameridhika ndani yenu, na kile ambacho Nataka kufanya kimetimia ndani yenu, bila makosa, wazi kabisa na kufichuliwa. Wale ambao wana nia mbaya na madhumuni—Nimeanza kuwaacha, na Nitafanya waanguke mmoja mmoja. Nitawaangamiza mmoja baada ya mwingine kufingia hatua ambapo wasiweze kuendelea kuishi—na haya yote yanarejelea roho zao, nafsi zao na miili yao.

Elewa kwamba kile ambacho mkono Wangu unafanya—kuwaruzuku maskini, kuwatunza na kuwalinda wale wanaonipenda Mimi, kuwaokoa wajinga na wenye raghba ambao hawaingilii kazi ya usimamizi Wangu, kuwaadhibu wale ambao hunipinga Mimi na wale ambao hawashirikiani Nami kikamilifu—mambo yote haya yatathibitishwa moja kwa moja kwa mujibu wa kile Nimesema tayari. Je, wewe ni mtu ambaye kwa kweli ananipenda Mimi? Je, wewe ni mtu ambaye kwa uaminifu hutumia rasilmali mwenyewe kwa ajili Yangu? Je, wewe ni mtu ambaye husikiliza neno Langu na kutenda ipasavyo? Je, wewe ni mtu ambaye hunipinga Mimi, au wewe ni mtu unayelingana na Mimi? Je, mawazo yako mwenye yako wazi juu ya mambo haya? Je, unaweza kujibu kwa mambo haya ambayo Nimeyasema moja kwa moja? Kama huwezi, wewe ni mtu ambaye hufuata kwa shauku, lakini hayaelewi mapenzi Yangu. Aina hii ya mtu kwa urahisi zaidi ataingilia usimamizi Wangu na kufikiria mapenzi Yangu visivyo. Iwapo mtu kama huyo kwa muda mfupi ana nia mbaya, yeye atafanyiwa uhamisho Wangu na maangamizo.

Ndani Yangu kuna mafumbo yasiyokuwa na mwisho, yasiyoweza kueleweka. Nitayafichua kwa watu moja kwa moja kulingana na mpango Wangu. Hiyo ni kwamba, Nitayafichua kwa wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume. Kwa wale ambao si waumini na ambao kunipinga Mimi, Nitawaruhusu kwenda na mkondo, lakini mwishowe lazima Niwafanye waelewe kwamba Mimi ni hukumu na uadhama. Watu wasioamini wa leo wanajua tu kinachotokea mbele ya macho yao, lakini hawajui mapenzi Yangu. Ni Wanangu wa kiume tu, ambao Nawapenda, wanaojua na kuelewa mapenzi Yangu. Kwa Wanangu wa kiume, Nimefichuliwa wazi wazi, lakini kwa Shetani Mimi ni hukumu na uadhama, sijafichwa hata kidogo. Leo ni wanangu wazaliwa wa kwanza wa kiume tu ambao wanastahili kujua mapenzi Yangu—hakuna mtu mwingine anayehitimu—na hili ndilo Nililopanga kabla ya uumbaji. Ni nani amebarikiwa na ni nani amepigwa mijeledi wote walikuwa wamepangwa vizuri nami mapema, Nilikuwa wazi kuhusu hili, na kwa sasa tayari limedhihirika kikamilifu: Wale waliobarikiwa wameanza kufurahia baraka zao, ilhali wale ambao wamechapwa viboko pia wameanza kuteseka kwa maafa. Wale ambao hawataki kuteseka na baa hata hivyo watateseka kwa sababu hili ndilo Nimeamua na hili ndilo mikono Yangu ya amri za kiutawala imepanga. Hasa ni aina gani ya mtu amebarikiwa na ni aina gani ya mtu amepigwa viboko? Tayari Nimefichua mambo haya; hili si siri kwenu, lakini limejitokeza waziwazi: Wale wanaonikubali Mimi lakini ambao nia zao ni mbaya; wale wanaonikubali Mimi lakini hawafuatilii; wale wanaonijua Mimi lakini si watiifu; wale wanaojiingiza katika uhalifu na udanganyifu kunihadaa Mimi; wale wanaosoma maneno Yangu lakini hutapika ukanaji; wale ambao hawajijui wenyewe, ambao hawajui wao ni nini, ambao wanajidhani kuwa wao wenyewe ni wakubwa, na ambao wanadhani kwamba wamefikia ukomavu (mfano wa Shetani), hawa ni vifaa vya baa. Wale ambao hunikubali Mimi na ambao nia yao ni kunielekea Mimi (na kama wakisababisha madakizo Mimi sitakumbuka makosa yao, lakini nia zao ni lazima ziwe za haki na ni lazima daima wawe na tahadhari, wawe makini na wasiwe wapotovu, na lazima daima waweke mioyoni mwao kunisikiliza Mimi na kunitii); wale ambao ni wasafi; wale ambao wako wazi; wale ambao ni waaminifu, wale ambao hawadhibitiwi na mtu yeyote, kitu, au jambo; watu walio kama watoto kwa kuonekana ingawa wao ni wakomavu katika maisha, hawa ndio wapendwa Wangu, vifaa vya baraka Yangu. Sasa, kila mmoja atachukua nafasi yake sahihi kwa mujibu wa hali yake. Na wewe utajua kama umebarikiwa au umepigwa viboko—hakuna haja Kwangu kusema dhahiri. Wale waliobarikiwa lazima washangilie na kuwa na furaha, huku wale ambao watafikwa na baa hawapaswi kuhuzunika. Yote mawili yamepangwa na mkono Wangu, lakini Mimi si wa kulaumiwa: Ni ukosefu wako mwenyewe wa ushirikiano hai na Mimi, na kushindwa kwako kuelewa kwamba Mimi ni Mungu anayetafuta ndani kabisa ya moyo wa binadamu; ni kile ambacho Nimeamua kabla, na ni kwa hila yako ndogo ambapo umejidhuru mwenyewe; ni kujiumiza mwenyewe! Kwamba lazima utumbukie Kuzimu si kutendewa vibaya! Huu ni mwisho wako; haya ni

matokeo yako!

Wabarikiwa wazaliwa wa kwanza wa kiume! Amkeni upesi kushangilia! Amkeni upesi kutoa sifa! Kuanzia sasa, hakutakuwa na uchungu zaidi, hakuna mateso tena, na kila kitu ki katika mikono yetu. Mtu yeyote ambaye anapatana nami ndiye Ninayempenda, na hatawekwa kwa mateso ya mabaa. Chochote ambacho ni hamu ya moyo wako, Nitakitimiza (lakini haiwezi kuwa kiholela), hii ni kazi Yangu.

Sura ya 70

Kwamba siri Zangu zinafichuliwa na zinadhihirika wazi, na hazifichiki tena, ni kwa sababu ya neema na rehema Zangu kabisa. Zaidi ya hayo, kwamba neno Langu linaonekana kati ya wanadamu, na halifichiki tena, nako pia ni kwa sababu ya neema na rehema Zangu. Ninawapenda wote wanaojitumia na kujitoa wenyewe kwa dhati kwa ajili Yangu. Nawachukia wale wote waliozaliwa kutoka Kwangu ila bado hawanijui Mimi, na hata wananipinga Mimi. Sitamwacha yeyote ambaye kwa dhati yuko kwa ajili Yangu; badala yake, baraka zake Nitazifanya ziwe mara dufu. Nitawaadhibu mara dufu wale wasio na shukrani na wanaokiuka fadhila Zangu, na sitawaachilia kwa urahisi. Katika ufalme Wangu hakuna upotovu au udanganyifu, na hakuna udunia; yaani, hakuna harufu ya wafu. Badala yake, yote ni unyofu na haki; yote ni usafi na uwazi, bila kuwa na chochote kilichofichika au kisicho wazi. Kila kitu ni kipya, kila kitu ni starehe, na kila kitu ni cha kujenga. Yeyote ambaye bado ananuka wafu hawezi kamwe kubakia katika ufalme Wangu, na badala yake atatawaliwa na fimbo Yangu ya chuma. Siri zote zisizo na mwisho, tangu zamani sana hadi sasa, zinafichuliwa kikamilifu kwenu—kundi la watu ambao wanapatwa na mimi katika siku za mwisho. Je, hamhisi kuwa mmebarikiwa? Zaidi ya hayo, siku ambazo yote yanafunuliwa wazi, ni siku ambazo mtashiriki utawala Wangu.

Kundi la watu ambao kwa kweli hutawala kama wafalme hutegemea majaliwa na uchaguzi Wangu, na kamwe hakuna mapenzi ya mwanadamu ndani yake. Yeyote anayethubutu kushiriki katika hili lazima apate pigo kutoka kwa mkono Wangu, na watu kama hao watakabiliwa na moto Wangu mkali; huu ni upande mwingine wa haki na uadhama Wangu. Nimeshasema kwamba ninatawala vitu vyote, mimi ndiye Mungu mwenye hekima ambaye ana mamlaka kamili, na Sina huruma kwa mtu yeyote; Mimi ni katili kabisa, sina hisia za kibinafsi kamwe. Ninamtendea mtu yeyote (haijalishi anaongea vizuri namna gani, Sitamwachilia) kwa haki, uadilifu na uadhama Wangu, wakati huohuo Nikimwezesha kila mtu kuona maajabu ya matendo Yangu vizuri zaidi, na vilevile maana ya matendo Yangu. Mmoja baada ya mwingine, Niliwaadhibu pepo wabaya kwa kila aina ya matendo wanayotenda, nikiwatupa kila mmoja ndani ya shimo lisilo na mwisho. Kazi hii Niliimaliza kabla ya wakati kuanza, nikawaacha bila

nafasi, nikiwaacha bila mahali pa kufanya kazi yao. Hakuna hata mmoja wa watu Wangu wateule—wale waliojaliwa na kuchaguliwa na Mimi—anayeweza kupagawa kamwe na roho waovu, na badala yake atakuwa mtakatifu daima. Lakini kwa wale ambao Sijawajalia na kuwachagua, Nitawakabidhi kwa Shetani, na sitaruhusu wabakie tena. Katika vipengele vyote, amri Zangu za kiutawala zinajumuisha haki Yangu na uadhama Wangu. Sitamwachilia hata mmoja wa wale ambao Shetani anatenda kazi kwao, lakini nitawatupa pamoja na miili yao kuzimuni, kwa maana namchukia Shetani. Sitamwachilia kwa urahisi hata kidogo, lakini nitamwangamiza kabisa, nisimruhusu hata fursa ndogo kabisa kufanya kazi yake. Wale ambao Shetani amewapotosha kwa kiwango fulani (yaani, wale ambao watakabiliwa na maafa) wako chini ya mpangilio wa hekima wa mkono Wangu. Msidhani kwamba hili limetokea kwa sababu ya ukali wa Shetani; jueni kuwa Mimi ni Mwenyezi Mungu anayetawala ulimwengu na vitu vyote! Kwangu Mimi, hakuna matatizo ambayo hayawezi kutatuliwa, sembuse kitu ambacho hakiwezi kukamilishwa au neno lolote ambalo haliwezi kusemwa. Wanadamu hawapaswi kutenda kama washauri Wangu. Jihadharini na kuangushwa na mkono Wangu na kutupwa kuzimuni. Nakuambia hili! Wale ambao wanashirikiana na Mimi leo kwa vitendo ndio werevu kupita wote, na wataepuka hasara na kukwepa maumivu ya hukumu. Yote haya ni mipangilio Yangu, iliyojaliwa na Mimi. Usitoe matamshi yasiyo na busara na usizungumze maneno matupu, ukidhani wewe ni mkuu sana. Je, yote haya hayatokani na majaliwa Yangu? Ninyi, ambao mnataka kuwa washauri Wangu, hamwoni aibu! Hamjui kimo chenu wenyewe; jinsi kilivyo kidogo kiasi cha kusikitisha! Hata hivyo, mnafikiri hili silo jambo kubwa, na hamjijui wenyewe. Tena na tena, mnayapuuza maneno Yangu, na kusababisha juhudi Zangu kubwa kuwa za bure na hamgundui hata kidogo kuwa ni udhihirisho wa neema na rehema Zangu. Badala yake, mnajaribu kuonyesha ujanja wenu tena na tena. Mnakumbuka hili? Je, ni adhabu gani ambayo watu ambao wanafikiri ni wajanja sana wanapaswa kupokea? Mkiwa wasiojali na wasio waaminifu kwa maneno Yangu, na msioyaandika mioyoni mwenu, mnanitumia Mimi kama kisingizio cha kufanya hivi na vile. Watenda mabaya! Je, ni lini ambapo mtaweza kuufikiria moyo Wangu kikamilifu? Hamuuzingatii, kwa hivyo kuwaita “watenda maovu” sio kuwatendea vibaya. Inawastahili kabisa!

Leo Ninawaonyesha, moja baada ya jingine, mambo ambayo zamani yalikuwa yamefichika. Joka kubwa jekundu limetupwa ndani ya shimo lisilo na mwisho na kuangamizwa kabisa, maana kuendelea kuliweka hakutakuwa na faida kabisa; hii inamaanisha kuwa haliwezi kumhudumia Kristo. Baada ya hapa, vitu vya rangi nyekundu havitakuwapo tena; hatua kwa hatua, lazima vipotee kabisa. Ninatenda kile Ninachosema; huku ndiko kukamilika kwa kazi Yangu. Ondoeni fikira za kibinadamu; kila kitu ambacho Nimesema, nimefanya. Yeyote anayejaribu kuwa mjanja hujiletea uangamizi na dharau, na hataki kuishi. Kwa hivyo, Nitakuridhisha, na hakika

sitawaweka watu kama hao. Baada ya hapa, idadi ya watu itaongezeka katika ubora, ilhali wote ambao hawashirikiana na Mimi kwa vitendo wataangamizwa kabisa. Wale ambao Nimewaidhinisha ndio ambao Nitawakamilisha, na sitamtupa hata mmoja. Hakuna ukinzani katika kile Ninachosema. Wale ambao hawashirikiani na Mimi kwa vitendo watapata adhabu zaidi, ingawa mwishowe, hakika nitawaokoa. Hata hivyo, kufikia wakati huo, kiwango cha maisha yao kitakuwa tofauti kabisa. Je, wewe unataka kuwa mtu kama huyo? Inuka na ushirikiane na Mimi! Hakika Sitamtendea vibaya yeyote anayejitumia kwa dhati kwa ajili Yangu. Kwa wale wanaojitolea Kwangu kwa bidii, Nitawapa baraka Zangu zote. Jitoe kikamilifu Kwangu! Kile unachokula, kile unachovaa, na siku zako zijazo vyote viko mikononi Mwangu; Nitapangilia kila kitu sawasawa, ili uwe na starehe isiyo na mwisho, ambayo hutaimaliza kamwe. Hii ni kwa sababu Nimesema, “Kwa wale ambao wanatumia rasilimali zao kwa ajili Yangu kwa dhati, hakika Nitakubariki sana.” Baraka zote zitakuja kwa kila mtu anayejitumia kwa dhati kwa ajili Yangu.

Sura ya 71

Mimi Nimejiweka mzima dhahiri kwenu, lakini kwa nini mnashindwa kutafakari maneno Yangu kwa mioyo na nafsi zenu zote? Kwa nini mnachukua maneno Yangu kama takataka? Je, Ninayosema ni makosa? Je, maneno Yangu yawakupiga katika sehemu ya uzima? Daima kuchelewesha, daima kusita, kwa nini mnafanya mambo hivi? Je, Mimi sijaongea wazi? Nimesema mara nyingi sana kwamba maneno Yangu lazima yatafakariwe kwa makini, na lazima yazingatiwe kwa makini. Je, kuna wowote kati yenu ambao ni watoto watiifu na wanyenyekevu? Je, Nimeongea bure? Je, hakuna matokeo kabisa? Ni kiasi gani cha yale yaliyo ndani yako yanayoweza kukidhi mapenzi Yangu? Kama, hata kama ni kwa muda, unashinda bila kukaripiwa, basi wewe utakuwa mpotovu na asiyedhibitika. Nisipoeleza wazi jinsi ya kutenda, au jinsi ya kuzungumza, je, inawezekana kwamba wewe huna wazo katika moyo wako? Nakwambia! Anayepata hasara ni yule ambaye ni mkaidi, ambaye hanyenyekei, ambaye anaamini kwa upofu! Kama mtu hawi makini kwa yale Ninayoyasema, kama hawezi kuelewa kila kitu, basi hataweza kuelewa nia Zangu, na hataweza kunitumikia Mimi. Mtu wa aina hii atashughulikiwa na Mimi, na atapambana na hukumu Yangu. Kutoelewa kila kitu ni kuwa fidhuli sana na kuwa na pupa kwa makusudi. Kwa hivyo Namchukia mtu wa aina hii, na Sina upole hata kidogo kwake, Simwonyeshi huruma yoyote ila uadhama wote na hukumu; ona kama bado unathubutu kunidanganya Mimi. Mimi ni Mungu ambaye huchunguza ndani kabisa ya moyo wa binadamu. Hoja hii yapaswa kuwa wazi kwa kila mtu; vinginevyo, wataendesha tu shughuli zao kwa njia ya kawaida na kunichukulia kwa njia isiyo ya dhati. Hii ndiyo sababu baadhi ya watu bila kujua hupigwa na Mimi. Nimesema kwamba Sitamshughulikia mtu yeyote pasi na haki, kwamba Sitafanya mambo maovu, kwamba kila kitu Nifanyacho ni kulingana na

mipango ya busara ya mkono Wangu.

Hukumu Yangu imeshuka juu ya watu wote wasionipenda kwa dhiti, wakati ambapo itakuwa wazi ni nani Niliyemjaalia na kumchagua, na ni nani ambao wameondolewa na Mimi. Haya sharti yawekwe wazi moja moja, bila kuficha chochote. Watu wote, matukio, na mambo yameasisiwa na yapo ili kuleta maneno Yangu kwa ukamilisho, na yanajishughulisha katika kufanya kweli maneno yaliyonenwa na kinywa Changu. Dunia na miisho ya ulimwengu vyote vinadhibitiwa na Mimi pekee. Lazima Nimpige yeyote anayethubutu kutoyatii maneno Yangu au kukataa kuyafanya matendo Yangu kuwa sheria, nikimfanya mtu huyo azame kuzimuni na akome kuishi. Maneno Yangu yote yanafaa na sahihi bila uchafu wowote. Je, kuzungumza kwenu kunaweza kufanana na Kwangu? Yote ni marefu na ya kuchosha, hueleweki na huelezi kwa dhahiri, na bado unafikiri umepata baadhi ya mambo, kwamba uko karibu sana. Nakwambia! Jinsi mtu alivyo mwenye kiburi zaidi, ndivyo anavyokuwa mbali na viwango Vyangu. Haonyeshi nadhari kwa mapenzi Yangu, naye hunidanganya Mimi na kuliaibisha jina Langu kwa ukali sana! Hana haya! Huangalii kimo chako mwenyewe. Wewe ni mpumbavu na mjinga kiasi ulioje!

Maneno Yangu huonyesha mambo wakati wote na katika sehemu zote. Je, inaweza kuwa kwamba bado huelewi, na bado huna uhakika? Je, unataka kunisikitisha Mimi? Jikakamue, na utayarishe ujasiri wako. Simtendei kwa ubaya mtu yeyote ambaye ananipenda Mimi. Mimi huchunguza ndani kabisa ya moyo wa binadamu na Najua yote ya yaliyo katika moyo wa kila mtu. Haya yote yatadhihirishwa moja moja, na yote yatapitia uchunguzi Wangu. Sitakosa kamwe kutotilia maanani mtu yeyote ambaye kwa kweli ananipenda Mimi. Wao wote ni wapokeaji wa baraka; wao ni kundi la wana wa kiume wazaliwa wa kwanza ambao Nimewajaalia kuwa wafalme. Na kwa wale ambao hawanipendi Mimi, wao ni madango ya hila zao wenyewe, na ni wapokeaji wa baa, na pia imejaaliwa na Mimi. Usihangaike. Nitawafichua mmoja mmoja. Nimeitayarisha kazi hii mapema kabla ya wakati, na Nimeanza kufanya kazi hii. Yote ni kwa mpango, si kwa machafuko kamwe. Tayari Nimemaliza kazi ya kuamua ni nani mteule na ni nani ameondolewa. Mmoja kwa mmoja watafichuliwa kwenu muone. Katika kipindi cha nyakati hizi mtaona kile mkono Wangu unachokifanya, watu wote wataona kwamba haki Yangu na uadhama Wangu haviruhusu kosa au upinzani kutoka kwa mtu yeyote, na kwamba mtu yeyote ambaye anakosea ataadhibiwa vikali.

Mimi Ndiye ambaye daima hukagua ndani kabisa ya moyo wa kila mtu. Msinione Mimi kutoka kwa nje tu. Wanadamu vipofu! Hamsikilizi maneno ambayo Nimeyazungumza wazi, na kabisa nyinyi hamniamini Mimi, ambaye ni Mungu Mwenyewe kamili. Bila shaka Sitamvumilia yeyote ambaye huthubutu kunirairai au kuficha chochote kutoka Kwangu.

Unakumbuka yale yote ambayo Nimesema? “Kuniona Mimi ni sawa na kuona kila moja ya siri iliyofichwa tangu milele hata milele.” Je, umeitafakari kwa makini taarifa hii? Mimi ni Mungu. Siri Zangu zimeonyeshwa wazi kwa ajili yenu. Je, hamjaziona? Kwa nini hamnizingatii? Na mbona unamwabudu Mungu asiye yakini ambaye yuko katika mawazo yako? Ningewezaje Mimi—Mungu mmoja wa kweli—kufanya kosa lolote? Lione hili kwa udhahiri! Kuwa na uhakika kwalo! Kila neno Langu na amali, kila tendo Langu na kila mwendo, kutabasamu Kwangu, kula Kwangu, na mavazi Yangu, kila kitu Changu hufanywa na Mungu Mwenyewe. Mnanihukumu Mimi; je, yawezekana kuwa kwamba tayari mlimwona Mungu kabla ya ujio Wangu? Hivyo kwa nini siku zote wewe hunilinganisha Mimi na Mungu wako katika moyo wako? Zote ni dhana za wanadamu! Vitendo Vyangu na tabia haviambatani na mawazo yako, sivyo? Huwa Simruhusu mtu yeyote kutoa maoni kama vitendo Vyangu na tabia ni sahihi au la. Mimi ndiye Mungu mmoja wa kweli. Huu ni ukweli usioweza kubadilishwa, na sahihi kabisa! Usidanganywe na hila zako mwenyewe. Maneno Yangu yamelisema kwa uwazi kabisa. Hakuna doa la ubinadamu ndani Yangu, na Mimi mzima ni Mungu Mwenyewe, Aliyedhihirishwa kikamilifu kwenu, bila kitu fiche!

Sura ya 72

Sharti unitegemee kuondoa upungufu ama udhaifu mara tu unapougundua. Usichelewe; vinginevyo kazi ya Roho Mtakatifu atakuwa mbali sana nawe, na utaanguka nyuma mbali sana. Kazi ambayo Nimekuaminia inaweza kutimizwa kwa kupitia tu kukaribia kwako mara kwa mara, kuomba, na kuwa na ushirika katika uwepo Wangu. Kama sivyo, hakuna matokeo yoyote yatakayofikiwa, na kila kitu kitakuwa bure. Kazi Yangu leo si kama ilivyokuwa awali. Kadiri ya maisha kwa watu Ninaowapenda si kama ilivyokuwa mbeleni. Wote wanayaelewa maneno Yangu kwa hakika, na wana umaizi mwelekevu juu yake. Hiki ndicho kipengele dhahiri kabisa; kinaweza zaidi kuakisi ajabu la kazi Yangu. Mwendo wa kazi Yangu unaongeza kasi, na kazi Yangu bila shaka ni tofauti na iliyopita. Ni vigumu kwa watu kudhania, na zaidi ya hayo ni vigumu kwa watu kuelewa. Hakuna kilicho fumbo kwenu tena; badala yake, kila kitu kinajulishwa na kujitokeza. Ni wazi, kinatolewa, na, hata zaidi, ni cha bure kabisa. Wale Ninaowapenda kwa hakika hawatazuiliwa na mtu yeyote, tukio, kitu, ama na kipindi ama jeografia; watavuka mipaka ya udhibiti unaotolewa na mazingira na wataibuka kutoka katika miili. Huu ndio ukamilisho wa kazi Yangu kuu. Hakutakuwa na yoyote itakayosalia; itakuwa imemalizika kabisa.

Ukamilisho wa kazi kuu unasemwa kwa kurejelea wazaliwa wote wa kwanza wa kiume na watu wote ambao Ninawapenda. Kuanzia sasa kuendelea hutadhibitiwa na mtu yeyote, tukio, ama kitu. Mtasafiri kotekote katika mataifa mbalimbali ya ulimwengu, mpite katika ulimwengu

mzima, ili kwamba nyayo zenu zisalie kila mahali. Msifikiri hili kuwa mbali sana; ni kitu ambacho kitatokea hivi punde mbele yenu. Kile Ninachokifanya kitaaminiwa kwenu, na pahali ambapo miguu Yangu itakanyaga patakuwa na nyayo zenu. Hii ndiyo maana ya kweli ya Mimi na nyinyi kutamalaki kama wafalme. Je, mmetafakari kwa nini ufunuo ambao Ninatoa daima u wazi zaidi, u dhahiri zaidi na zaidi, pasipo kufichwa hata kidogo? Kwa nini Nimeshuhudia ushuhuda mkuu zaidi, na kuwaambia kuhusu mafumbo yote na maneno yote? Sababu si nyingine ila kazi ambayo imetajwa hapo juu. Maendeleo ya kazi yenu kwa sasa ni ya polepole sana, hata hivyo. Hamna uwezo wa kuenda kwa mwendo sawa na Ninavyopiga hatua, hamwezi kushirikiana na Mimi vyema zaidi, na kwa sasa bado hamna uwezo wa kutimiza mapenzi Yangu. Lazima Niwafunze kwa nguvu zaidi, Nizidishe kasi ya ukamilisho Wangu kwenu, ili kuwaruhusu kuuridhisha moyo Wangu haraka iwezekanavyo.

La wazi zaidi sasa ni kwamba kundi la wazaliwa wa kwanza limeundika kabisa, wote wakiidhinishwa na Mimi, ambao walikuwa hata wameamuliwa kabla na kuchaguliwa na Mimi tangu uumbaji wa dunia, kila mmoja akikuzwa na mkono Wangu mwenyewe. Hakuna nafasi ya kufikiria kwa mwanadamu katika hili, na haliwezi kudhibitiwa nawe. Usijivune; yote ni ukarimu Wangu na huruma. Machoni Pangu, kila kitu tayari kimetimizwa. Ni kwa sababu tu macho yenu yana ukungu, na hata sasa huwezi kuona wazi ajabu la vitendo Vyangu. Hamko wazi kikamilifu na hamuelewi kabisa kuhusu kudura Yangu, hekima Yangu, kila kitendo Changu, na kila neno Langu na tendo. Kwa hivyo Nazungumza dhahiri. Kwa wana Wangu, wapendwa Wangu, Niko radhi kulipa gharama, Niko radhi kufanya kazi kwa bidii, na Niko radhi kujitumia Mwenyewe. Je, unanijua kupitia kwa maneno Yangu? Je, unahitaji kwamba Niseme wazi zaidi? Usiwe mpotovu tena; fikiri juu ya moyo Wangu! Sasa kwa kuwa fumbo kuu limefumbuliwa kwenu, mna lipi la kusema? Je, bado mna malalamiko yoyote? Msipolipa thamana na kutia bidii, je, mnaweza kustahili shida yote ambayo Nimepitia?

Siku hizi watu hawawezi kujidhibiti. Nisipompendelea mtu, hataweza kunipenda, ingawa anaweza kutaka kufanya hivyo. Watu ambao Nimewajaalia na kuwachagua, hata hivyo, hawataweza kuepuka ingawa wangetaka kufanya hivyo; bila kujali popote waendapo hawataweza kuepuka kiganja cha mkono Wangu. Hivyo ndivyo ulivyo uadhama Wangu, hata zaidi ilivyo hukumu Yangu. Watu wote sharti wafanye shughuli zao kulingana na mpango Wangu, na kulingana na mpenzi Yangu. Kila kitu kutoka hapa hadi nje hurejea mikononi Mwangu kabisa, na hawawezi kukidhibiti wenyewe. Kimedhibitiwa na Mimi kikamilifu, kimepangwa na Mimi. Mtu asiposhiriki kwa kiasi kidogo, Sitamwacha aende kwa urahisi. Kuanzia leo, Nitawaruhusu watu wote waanze kunijua—Mungu wa pekee wa kweli aliyeviumba vyote, aliyekuja miongoni mwa watu na kukataliwa na kukashifiwa nao, anayedhibiti na kupanga kila kitu, mfalme anayesimamia ufalme, Mungu Mwenyewe anayesimamia ulimwengu, hata

zaidi Mungu anayedhibiti maisha na mauti ya watu, mwenye ufunguo wa Kuzimu. Nitawaruhusu watu wote (wazima, watoto, bila kujali ikiwa wana roho au la, ama ikiwa ni wapumbavu ama walemavu, nk.) wanijue. Simwachilii yeyote kutoka kwa kazi hii; ni kazi inayohitaji ustadi kabisa, kazi ambayo Nimetayarisha vema, kazi ambayo inatekelezwa kuanzia sasa hivi. Ninalosema litafanyika. Yafungue macho yako ya Kiroho, ziache dhana zako, na utambue kuwa Mimi ndimi Mungu wa kweli wa pekee Anayetawala ulimwengu! Sijafichwa kwa yeyote, na Mimi hutekeleza amri Zangu za utawala kwa kila mtu.

Viweke kando vitu vyako vyote. Je, si vitu vyote unavyovipata kutoka Kwangu ni vya thamani kubwa na vyenye umuhimu mkuu? Je, hakuna tofauti kubwa mno kati ya hayo na takataka yako? Usipoteze wakati wowote katika kuviacha vitu vyote vya bure! Imeamuliwa sasa iwapo baraka zinapatikana ama kukumbana na msiba. Sasa ni wakati muhimu; hata zaidi ni wakati wa umakinifu. Je, unaweza kuona hili?

Sura ya 73

Maneno Yangu yanatimizwa mara tu yanaposemwa; hayabadiliki kamwe na ni sahihi kabisa. Kumbuka hili! Kila neno na kirai kutoka katika kinywa Changu lazima yafikiriwe kwa uangalifu. Kuwa makini zaidi, usije ukapitia upotezaji na kupokea hukumu Yangu, ghadhabu Yangu na moto Wangu pekee. Kazi yangu sasa inasonga mbele kwa kasi ya haraka sana, ingawa si ya haraka haraka; imesafishwa kwa ustadi sana kwamba haiwezi kabisa kuonekana kwa macho tu, na haiwezi kushikwa na mikono ya wanadamu. Ni iliyofanywa kwa uangalifu hasa. Mimi huwa Sitamki maneno matupu; kila Ninachosema ni kweli. Unapaswa kuamini kwamba kila neno ni la kweli na sahihi. Usiwe mzembe; huu ni wakati muhimu! Ikiwa utapata baraka au bahati mbaya itaamuliwa katika wakati huu hasa, na tofauti iko hivyo kati ya mbingu na dunia. Iwapo unaenda mbinguni au Kuzimuni yote iko katika udhibiti Wangu kikamilifu. Wale wanaokwenda Kuzimuni wanajihusisha na mapambano yao ya mwisho ya kufa, wakati wale wanaoenda mbinguni wanapitia mateso yao ya mwisho na kutumika kwao kwa mwisho kwa ajili Yangu, na kila kitu wanachofanya katika siku zijazo ni kufurahia na kusifu, bila vitu vyote visivyo vya maana vinavyowasumbua watu (ndoa, kazi, utajiri wenye kukera, hadhi, na kadhalika). Lakini kwa wale wanaoenda Kuzimuni, mateso yao ni ya milele (hii inahusu roho, nafsi, na mwili wao), kamwe wasitoroke kutoka kwa mkono Wangu wa adhabu. Pande hizi mbili hazipatani kama moto na maji. Hakuna kutatizana: Wale wanaopatwa na bahati mbaya wataendelea kupatwa na bahati mbaya, wakati wale waliobarikiwa watafurahia hadi watosheke.

Matukio yote na vitu vinadhibitiwa na Mimi, bila kutaja kwamba ninyi—wanangu, wapendwa Wangu—ni Wangu hata zaidi. Ninyi ndio dhihirisho la mpango Wangu wa usimamizi wa miaka 6,000, hazina Zangu. Wale wote Ninaowapenda wanapendeza macho Yangu, kwa

sababu wananidhihirisha; wale wote Ninaowachukia Ninawadharau bila hata kuwatazama, kwa sababu wao ni wazawa wa Shetani na ni wa Shetani. Leo, kila mtu anapaswa kujichunguza mwenyewe: Kama nia zako ni sahihi na unanipenda kwa kweli, basi hakika utapendwa na Mimi. Lazima unipende kweli na lazima usinidanganye! Mimi ni Mungu anayechunguza ndani zaidi ya mioyo ya watu! Kama nia zako ni mbaya na wewe ni baridi na usiye mwaminifu Kwangu, basi bila shaka utachukiwa na Mimi na hukuwa umechaguliwa au kuamuliwa kabla na Mimi. Wewe subiri tu kwenda kuzimu! Watu wengine wanaweza kukosa kuona mambo haya, lakini ni wewe tu na Mimi—Mungu anayetazama kwa kina ndani ya mioyo ya wanadamu—tunaoyajua. Yatafichuliwa kwa wakati fulani. Waaminifu hawahitaji kuwa na wasiwasi na wasio waaminifu hawahitaji kuwa na hofu. Yote ni sehemu ya mpango Wangu wa hekima.

Kazi hii ni ya dharura na nzito, na inawahitaji kutumia kwa ajili Yangu mara moja ya mwisho kukamilisha kazi hii ya mwisho. Mahitaji Yangu siyo ya juu: Nawahitaji tu kuweza kuratibu nami vizuri sana, kuniridhisha katika kila kitu, kufuata uongozi Wangu ndani yenu. Msiwe vipofu; muwe na lengo, na kuhisi nia Zangu kutoka kwa kila kipengele na katika kila kitu. Hii ni kwa sababu Mimi si Mungu aliyefichwa kwenu tena. Lazima muwe wazi sana juu ya hili ili muelewe nia Zangu. Katika muda mfupi sana, hamtakutana tu na wageni wanaotafuta njia ya kweli, kilicho cha muhimu zaidi ni kwamba ninyi mnapaswa kuwa na uwezo wa kuwaongoza. Hiyo ndiyo nia Yangu ya dharura. Haikubaliki iwapo hamwezi kuona hili. Hata hivyo, lazima uamini katika kudura Yangu. Mradi tu watu wako sahihi, hakika Nitawafundisha kuwa askari wema. Kila kitu kimepangwa na Mimi ipasavyo. Lazima mtamani kuteseka kwa ajili Yangu. Huu ndio wakati muhimu. Msiukose! Sitakumbuka mambo kutoka katika siku zenu za nyuma. Lazima uombe na kusihi mbele Zangu mara nyingi; Mimi Nitakupa neema ya kutosha kwa furaha na matumizi yako. Neema na baraka si kitu kimoja. Kile mnachofurahia sasa ni neema Yangu na hakifai kutajwa machoni Pangu, ilhali baraka ni kile mtakachofurahia milele katika siku zijazo. Hizo ni baraka ambazo watu hawajafikiria na hawawezi kufikiria. Nasema mmebarikiwa kwa sababu hii—ni baraka ambayo mwanadamu hajafurahi tangu uumbaji.

Tayari Nimefichua yote Yangu kwenu. Natumaini tu kwamba ninyi mtakuwa wenye huruma kwa moyo Wangu, kufikiria kwa ajili Yangu katika kila jambo, na kuwa wenye huruma Kwangu katika kila kitu, ili kila Ninachoona kila mara ni nyuso zenu zenye kutabasamu. Kuanzia sasa kuendelea, wale wanaopata hadhi ya wazaliwa wa kwanza ni watu ambao watatawala kama wafalme pamoja nami. Hawatadhulumiwa na ndugu yeyote, wala hawataadibiwa au kushughulikiwa na Mimi, kwa sababu kanuni Yangu ya kufanya mambo ni: Wale walio katika kikundi cha wazaliwa wa kwanza ni watu wanaodharauliwa na kudhulumiwa na wengine na wamepitia mabadiliko yote ya maisha. (Wameshughulikiwa na kuvunjwa na Mimi mapema, na wamefanyika wakamilifu mbeleni.) Watu hawa tayari wamefurahia pamoja na

Mimi baraka wanazopaswa kupokea mapema. Mimi ni mwenye haki na Simpendelei yeyote.

Sura ya 74

Wamebarikiwa wale ambao wamelisoma neno Langu na kuamini kwamba litatimizwa—Sitakutendea vibaya, lakini Nitafanya yale unayoamini yatimizwe kwako. Hii ni baraka Yangu ikija kwako. Neno Langu linapiga siri zilizofichwa ndani ya kila mtu. Kila mtu ana majeraha ya mauti, na Mimi ni tabibu mzuri ambaye anayaponya—njoo tu katika uwepo Wangu. Kwa nini Nilisema kuwa katika siku zijazo hakutakuwa na huzuni tena na hakutakuwa na machozi tena? Ni kwa sababu ya hili. Ndani Yangu, kila kitu kinatimizwa, lakini ndani ya wanadamu, vitu vyote ni vipotovu na bure, na vyote ni vidanganyifu kwa wanadamu. Katika uwepo Wangu utapokea vitu vyote, na utaona na pia kufurahia baraka zote ambazo hungewahi kufikiria. Wale wasiokuja mbele Yangu bila shaka ni waasi, na hakika ndio wanaonipinga Mimi. Hakika Sitawaacha kwa urahisi; Nitamwadibu vikali mtu wa aina hii. Kumbuka hili! Wale wanaokuja mbele Yangu zaidi watapata zaidi, lakini haitakuwa zaidi ya neema. Baadaye, watapata baraka nyingi hata zaidi.

Tangu uumbaji wa ulimwengu Nimeanza kuamulia kabla na kuchagua kundi hili la watu, yaani, ninyi leo. Tabia yako, ubora wa tabia, sura, kimo, familia ambayo ulizaliwa kwayo, kazi yako na ndoa yako, nafsi yako yote, hata rangi ya nywele yako na ngozi yako, na wakati wa kuzaliwa kwako vyote vilipangwa na mikono Yangu. Hata mambo unayofanya na watu unaokutana nao kila siku hupangwa na mikono Yangu, sembuse ukweli kwamba kukuleta katika uwepo Wangu leo kwa kweli ni mpango Wangu. Usijitupe katika vurugu; unapaswa kuendelea kwa utulivu. Kile Ninachokuruhusu kufurahia leo ni mgawo ambao wewe unastahili, na Nilikipangia kabla katika uumbaji wa dunia. Wanadamu wote ni waliozidi sana—wao huwa vichwa ngumu sana au wasio na aibu kabisa. Hawawezi kufanya mambo kulingana na mpango Wangu na mpangilio. Usifanye hilo tena. Ndani Yangu vyote vinakombolewa; usijifunge mwenyewe, kwani utayapoteza maisha yako. Kumbuka hili!

Amini kwamba kila kitu kiko mikononi Mwangu. Yale yaliyochukuliw kuwa siri kwenu katika siku za nyuma yote yanafichuliwa wazi leo; hakijafichika tena (kwa maana Nimesema kuwa katika siku za baadaye hakuna kitu kitakachobaki kikiwa kimefichika). Watu huwa bila subira mara nyingi; wao wana hamu sana ya kukamilisha kitu fulani na hawafikirii yaliyo ndani ya moyo Wangu. Nawafundisha ili muweze kushiriki mzigo Wangu na kusimamia nyumba Yangu. Nataka mkue kwa haraka ili muweze kuwaongoza ndugu zenu ambao ni wadogo kuliko ninyi, ili sisi Baba na wana tuweze kuunganishwa tena karibuni na kamwe hatutatengwa. Hii itaridhisha hamu ya moyo Wangu. Fumbo tayari limefichuliwa kwa watu wote, na hakuna chochote kinachobaki kikiwa kimefichika: Mimi—Mungu mkamilifu Mwenyewe, aliye na

ubinadamu wa kawaida na uungu kamili—Nimefichuliwa mbele ya macho yenu leo. Nafsi Yangu nzima (mavazi, sura ya mwili, na umbo la mwili) ni dhihirisho kamili la Mungu Mwenyewe, na ni nafsi ya Mungu ambayo wanadamu wamewazia tangu kuumbwa kwa ulimwengu lakini ambayo hakuna mtu ameiona. Sababu ya vitendo Vyangu kuwa vizuri kama maneno Yangu ni kwamba ubinadamu Wangu wa kawaida na uungu kamili hukamilishana; aidha hili huwawezesha watu wote kuona kwamba mtu wa kawaida anashikilia nguvu kuu sana kama hiyo. Wale kati yenu ambao mnaniamini kweli hufanya hivyo kwa sababu Nilikupa moyo wa kweli ili kukuwezesha kunipenda. Ninapokushughulikia, Ninakumulikia na kukupa nuru na kukuruhusu kunijua kupitia kwa hilo. Kwa hiyo, bila kujali jinsi Ninavyokushughulikia, hutatoroka. Badala yake, utakuwa na uhakika na Mimi zaidi na zaidi. Wakati wewe ni dhaifu, pia ni mpangilio Wangu, ambao unakuwezesha kuona kwamba punde unaponiacha Mimi utakufa na kunyauka. Kutokana na hilo unaweza kujua kwamba Mimi ndimi uhai wako. Unavyokuwa na nguvu baada ya kuwa dhaifu, litakuruhusu kuona kwamba kuwa dhaifu au mwenye nguvu hakukutegemei, lakini kunanitegemea Mimi kabisa.

Mafumbo yote yanafichuliwa kabisa. Katika shughuli zenu za baadaye, Nitawapa maagizo Yangu, katika kazi baada ya kazi. Nitakuwa dhahiri kabisa; Nitakuwa wazi kabisa na hata kuzungumza nanyi moja kwa moja ili msihitaji kutafakari kuyahusu wenyewe, msije mkakatiza usimamizi Wangu. Ndiyo maana Mimi mara kwa mara Nasisitiza kwamba baadaye hakutakuwa na kingine tena ambacho kimefichika.

Sura ya 75

Yote yatatimizwa punde tu maneno Yangu yanapozungumzwa, bila kupotoka hata kidogo. Kuanzia sasa kwendelea, mafumbo yote yaliyofichwa hayatazuiwa au kufunikwa hata kidogo, na yatafichuliwa kwenu—wanangu wapendwa. Nitakufanya uone hata ishara na maajabu kubwa zaidi ndani Yangu, na kuona hata mafumbo makubwa zaidi. Mambo haya hakika yatawashangaza na kuwapa ufahamu bora zaidi wa Mimi, mwenyezi Mungu, na kuwaruhusu kufahamu hekima Yangu humo. Leo ninyi mnaletwa uso kwa uso na Mungu mmoja wa kweli ambaye wanadamu hawajawahi kumwona tangu uumbaji, na hakuna kitu maalum kunihusu Mimi. Ninakula, kuishi, kuzungumza na kucheka na nyinyi, na daima Ninaishi ndani yenu, wakati huo huo pia Nikisonga miongoni mwenu. Kwa wale ambao hawaamini au ambao wana mawazo yao wenyewe ya kusikitisha, hiki ni kizuizi. Hii ni hekima Yangu. Nitawafichulia pia watu wengine juu ya vitu ambavyo ubinadamu Wangu wa kawaida haujui, lakini hili halimaanishi kwamba Mimi si Mungu Mwenyewe. Kinyume chake, hoja hii inatosha kuthibitisha kwamba Mimi ni mwenyezi Mungu. Kwa watu wanaoamini, hoja hii ina athari ya maamuzi, na kwa sababu ya hoja hii tu, wao wana uhakika wa asilimia mia moja Kwangu.

Msiwe na hamu kupita kiasi; Nitawafichulia vitu kimoja baada ya kingine.

Kwa ajili yenu, Mimi ni wazi na Sijajificha. Hata hivyo, kwa ajili ya wasioamini—wale walio wadanganyifu, ambao wamepotoshwa na Shetani kwa kiwango fulani—Nitabaki Nimejificha. Hata hivyo, Nilipozungumzia awali kuhusu kujifichua kwa watu wote, Nilikuwa nikirejelea haki Yangu, hukumu Yangu, na utukufu Wangu, ili kuwa wangejua kutokana na matokeo wanayopokea kwamba Mimi ni msimamizi wa ulimwengu na vitu vyote. Tendeni kwa ujasiri! Kuweni watulivu tu! Usiogope: Mimi—Baba yenu—niko hapa kuwasaidia na hamtateseka. Alimradi muombe na kusali zaidi mbele Yangu mara kwa mara, Nitawapa imani yote. Kutoka kwa nje, wale walio na mamlaka wanaweza kuonekana kuwa waovu, lakini msiogope, kwa kuwa hii ni kwa sababu mna imani kidogo. Almuradi imani yenu ikue, hakuna kitu kitakachokuwa kigumu mno. Rukeni kwa furaha hadi mridhike sana! Kila kitu ki chini ya miguu yenu, na ndani ya mshiko Wangu. Je, si mafanikio au maangamizo hayaamuliwi na neno Langu moja tu?

Wale wote ambao Ninawatumia sasa Niliwakubali zamani, mmoja baada ya mwingine. Yaani, wale watu katika kikundi cha wazaliwa wa kwanza wameshaamuliwa, na wameamuliwa tangu Nilipoumba ulimwengu huu. Hakuna anayeweza kubadilisha hili, na vyote lazima viamrishwe na Mimi. Hakuna binadamu anayeweza kufanya hivyo; hii yote ni mipangilio Yangu. Nikiwepo, kila kitu kitakuwa thabiti na salama; Nikiwepo, vyote vitafanywa kwa usahihi na vizuri, bila kutumia jitihada hata kidogo. Ninasema na yanatendeka; Ninazungumza na yanafanywa. Hali ya kimataifa ikiwa katika msukosuko, kwa nini hamjakimbia kuanza mafunzo yenu? Mtangoja hadi lini? Je, mtasubiri mpaka ile siku ambayo wageni watafurika nchini China kukutana na nyinyi? Huenda mlikuwa goigoi kidogo hapo awali, lakini hamwezi kuendelea kujifurahisha! Wanangu! Kuweni wenye kufikiria nia Zangu za bidii! Wale ambao wanakaribia mara nyingi zaidi watapata kila kitu. Je, hamniamini?

Kasi ya kazi Yangu ni mwali wa umeme, lakini hakika si sauti ingurumayo ya radi. Je, mnaelewa maana halisi ya maneno haya? Lazima muwe na uwezo wa kuratibu vyema zaidi na Mimi na kuwa wenye kufikiria nia Zangu. Mnataka kupokea baraka, lakini pia mnaogopa mateso; hii si hisia yenu kinzani? Hebu Nikwambie! Kama mtu anatamani kupokea baraka leo lakini hajitolei kila kitu kuhusiana na hilo, basi yote atakayopokea ni adhabu na hukumu Yangu. Hata hivyo, wale wanaojitolea kila kitu watapata amani katika kila kitu na kuwa na kila kitu kwa wingi, na kila kitu wanachopokea kitakuwa baraka Zangu. Kinachohitajika kwa dharura leo ni imani yenu, na kwenu kulipa gharama. Msitafsiri visivyo nia Zangu. Kila kitu kitakuja kutimia, na mtakiona kwa macho yenu wenyewe na kukipitia ninyi wenyewe. Nikiwepo, hakuna neno hata moja lisilo kweli au la uongo; kila kitu Ninachosema ni ukweli kabisa, na hakikosi hekima.

Msiamini nusu na kushuku nusu. Mimi ndimi Ninayekamilisha kila kitu miongoni mwenu, na Mimi pia ndimi Ninayehukumu na kuwashughulikia wale wanaofanya maovu. Ninawapenda, na ninawafanya muwe wakamilifu. Kwao, hata hivyo, Mimi ni kinyume kabisa: chuki na uharibifu, bila ya uhuru wa kuwa na fikira tofauti na bila kuacha alama. Wingi Wangu ni wa asili katika kila kitu Ninachosema na kufanya. Je, mmevichunguza kidogo kidogo? Maneno mengine Nimeyasema mara nyingi, basi kwa nini hamwelewi kile Ninachomaanisha? Baada ya ninyi kusoma Maneno Yangu, je, kila kitu kitakuwa kama vile kinavyopaswa kuwa? Je, kila kitu basi kinafanikishwa? Hamna nia yoyote ya kufikiria moyo Wangu. Kwa nini Nasema kuwa Mimi ni Mungu mmoja wa kweli mwenye mamlaka kamili, mwenye kudura ambaye anaangalia ndani sana ya mioyo ya watu? Je, bado hamwelewi maana ya maneno haya? Je, umekariri kila neno Niliyosisitiza Je, yamekuwa kwa kweli kanuni za jinsi unavyotenda?

Ninasimama juu ya kila kitu, Nikiutazama ulimwengu wote. Nitaonyesha nguvu Zangu kuu na hekima Yangu yote kwa kila taifa na watu. Msifanye tu kila mnachoweza kufuatilia raha hivi sasa. Wakati mataifa yote ya ulimwengu yanaungana, ni kitu gani ambacho hakitakuwa chenu? Hata hivyo, Sitawaacha mpungukiwe sasa, wala Sitawaacha mteseke. Amini kwamba Mimi ni mwenyezi Mungu! Kila kitu kitafanikishwa na kuwa bora zaidi na zaidi! Wazaliwa Wangu wa kwanza! Baraka zote zitawajia! Ninyi mtazifurahia bila kukoma, zisizopungua katika ugavi, zilizojaa na za wingi, na zilizojaa kikamilisho!

Sura ya 76

Matamshi Yangu yote ni maonyesho ya mapenzi Yangu. Ni nani anayeweza kuudhukuru mzigo Wangu? Nani anayeweza kuelewa nia Yangu? Je, mmefikiria kila moja ya maswali Niliyoibua kwenu? Uzembe ulioje! Unathubutu vipi kuvuruga mipango Yangu? Wewe Wewe umevuka mipaka! Kazi kama hii ya pepo wabaya ikiendelea, Nitawatupa mautini mara moja katika shimo lisilo na mwisho! Kwa muda mrefu Nimeona waziwazi matendo mbalimbali ya pepo wabaya. Na watu wanaotumiwa na pepo wabaya (wale wenye nia mbaya, wale wanaotamani mwili au utajiri, wale wanaojikuza, wale wanaolivuruga kanisa, nk.) kila mmoja wao pia amebainika na Mimi. Usifikiri kwamba kila kitu kimemalizika punde pepo wabaya watatupwa nje. Hebu Nikwambie! Kuanzia sasa na kuendelea, Nitawaondoa watu hawa mmoja baada ya mwingine, nisiwatumie kamwe! Yaani, mtu yeyote aliyepotoshwa na pepo wabaya hatatumiwa na Mimi, na atafukuzwa! Usifikiri kuwa Sina hisia! Fahamu jambo hili! Mimi ndimi Mungu mtakatifu, na Sitakaa katika hekalu chafu! Mimi huwatumia tu watu waaminifu na wenye hekima ambao ni waaminifu kabisa Kwangu na wanaoweza kuudhukuru mzigo Wangu. Hii ni kwa sababu watu kama hao walijaaliwa na Mimi, na bila shaka hakuna pepo wabaya wanaowafanyia kazi hata kidogo. Hebu Nieleze wazi jambo moja: Kuanzia sasa na kuendelea,

wale wote ambao hawana kazi ya Roho Mtakatifu wana kazi ya pepo wabaya. Hebu Nirudie: Simtaki hata mtu mmoja ambaye pepo wabaya humfanyia kazi. Wote watatupwa kuzimuni pamoja na miili yao!

Matakwa Yangu kwenu hapo zamani yalikuwa malegevu kidogo, na mmekuwa wapotovu inapohusu mwili. Kuanzia siku hii na kuendelea, Sitawaruhusu mwendelee hivi. Ikiwa maneno na vitendo vyako havinidhihirishi katika kila namna, au kama haviko katika mfano Wangu hata kidogo, basi bila shaka Sitawasamehe kwa urahisi. Vinginevyo, mngekuwa mkicheka na kufanya utani kila mara, mkivunja mbavu zenu kwa vicheko, bila kizuizi chochote. Unapotenda jambo baya, je, huhisi kuwa Nimekuacha? Kwa kuwa unajua, kwa nini bado u mpotovu? Je, bado unasubiri mguso wa mkono Wangu wa hukumu? Kuanzia leo, Nitamwadhibu mara moja mtu yeyote asiyekubaliana na nia Yangu hata kwa wakati mmoja. Mkikaa pamoja mkipiga umbeya, basi Nitakuacha. Usizungumze ikiwa hutoi ruzuku ya kiroho. Sisemi hivi ili kuwazuia, lakini Ninamaanisha kwamba kwa kuwa kazi Yangu imeendelea hadi hatua iliyopo sasa, Nitaendelea mbele kulingana na mpango Wangu. Mkiketi pamoja mkiwasiliana kuhusu mambo ya kiroho katika maisha, basi Nitakuwa pamoja nanyi. Sitamtendea yeyote kati yenu pasi na haki. Ukifungua kinywa chako, Nitakupa maneno yanayofaa. Unapaswa kufahamu moyo Wangu kutoka ndani ya maneno Yangu. Siwaambii mjifanye kuwa bubu, wala Siwaambii mshiriki katika porojo.

Kwa nini Ninaendelea kusema kwamba hakuna muda mwingi uliobaki, na kwamba siku Yangu haipaswi kucheleweshwa? Je, mmefikiria kuhusu jambo hili kwa makini? Je, mnaelewa maana ya maneno Yangu kweli? Yaani, Nimekuwa nikifanya kazi tangu nilipoanza kuzungumza. Kila mmoja wenu amekuwa lengo la kazi Yangu, si mtu yeyote hasa; na zaidi ya hayo, si mtu mwingine yeyote. Mna wasiwasi tu kuhusu kutofurahia baraka, lakini hamfikirii juu ya maisha yenu. Ninyi ni wapumbavu kweli! Mnasikitisha sana! Hamuufikirii mzigo Wangu hata!

Juhudi Zangu zote za mchwa na gharama ambayo Nimelipa vimekuwa kwa ajili yenu. Ikiwa hamuufikirii mzigo Wangu, basi hamjafikia matarajio Yangu kwa ajili yenu. Mataifa yote yanawasubiri mmiliki, na watu wote wanawasubiri mtawale. Nimeweka kila kitu mikononi mwenu. Sasa, wale wote walio mamlakani wameanza kujiuzulu na wameanguka, na wanasubiri tu hukumu Yangu iwafike. Angalia waziwazi! Dunia inaanguka sasa, huku ufalme Wangu umejengwa kwa mafanikio. Wanangu wameonekana na wazaliwa Wangu wa kwanza wanatawala pamoja na Mimi kama wafalme, wakitawala mataifa na watu mbalimbali. Usifikiri hili ni jambo lisilo yakini; ni ukweli ulio dhahiri. Je, sivyo? Mara tu mtakapoomba na kunisihi, Nitachukua hatua mara moja na kuwaadhibu wale wanaowatesa, kuwashughulikia wale

wanaowasumbua, kuwaharibu wale mnaowachukia, na kuwatawala watu hao, matukio, na vitu ambavyo huwatumikia. Nimesema mara nyingi: Sitamletea wokovu mtu yeyote anayemtumikia Kristo (yaani, mtu yeyote ambaye hutoa huduma kwa Mwanangu). Kumhudumia Mwanangu hakumaanishi kuwa wao ni watu wema; ni kutokana na nguvu Zangu kuu na matendo ya ajabu tu. Msitilie umuhimu sana katika binadamu. Hakika watu kama hao hawana kazi ya Roho Mtakatifu na hawaelewi mambo ya kiroho kabisa. Hawatakuwa na manufaa yoyote baada ya Mimi kumaliza nao. Kumbuka hili! Huu ni uthibitisho Wangu kwenu. Msielewe tu bila mpango, mnafahamu?

Kuna watu wachache zaidi na zaidi, lakini washiriki wanazidi kusafishwa zaidi na zaidi. Hii ni kazi Yangu, mpango Wangu wa usimamizi, na zaidi ya hayo hekima Yangu na kudura Yangu. Ni uratibu wa ubinadamu Wangu wa kawaida na uungu Wangu kamili. Je, mnaona jambo hili waziwazi? Je, mna ufahamu wowote wa kweli kuhusu jambo hili? Nitatimiza moja baada ya lingine, kupitia uungu Wangu, kila kitu ambacho Nimenena kutoka kwa ubinadamu Wangu wa kawaida. Hii ndiyo sababu Ninaendelea kusema kuwa kile Ninachosema kitafanyika bila ya utata wowote; badala yake, yote yatakuwa wazi na dhahiri sana. Kila kitu Ninachosema kitatimizwa, na hakika hakitatendeka ovyoovyo. Sizungumzi maneno matupu na Sifanyi makosa. Yeyote atakayethubutu kunipima atahukumiwa, na hakika hataweza kuponyoka kiganja cha mkono Wangu. Mara maneno Yangu yanapozungumzwa, ni nani anayethubutu kupinga? Ni nani anayethubutu kunirairai au kunificha chochote? Nimesema hapo awali: Mimi ni Mungu mwenye hekima. Ninatumia ubinadamu Wangu wa kawaida kuwafichua watu wote na tabia ya shetani, kuwafichua wale wenye nia mbaya, wale wanaotenda kwa njia moja mbele ya wengine na kwa njia nyingine bila wao kufahamu, wale wanaonipinga, wale wasio waaminifu Kwangu, wale wanaotamani fedha, wale ambao hawaudhukuru mzigo Wangu, wale wanaojihusisha na ulaghai na udanganyifu pamoja na ndugu zao, wale wanaozungumza kwa maneno matamu ili kuwafanya watu wafurahi, na wale ambao hawawezi kuratibu na ndugu zao kwa umoja kwa kujitolea. Kwa sababu ya ubinadamu Wangu wa kawaida, watu wengi sana hunipinga kwa siri na kushiriki katika ulaghai na udanganyifu, wakidhani kuwa ubinadamu Wangu wa kawaida haujui. Na watu wengi sana wanatilia maanani maalum ubinadamu Wangu wa kawaida, wakinipa vitu vizuri nile na kunywa, wakinitumikia kama watumishi, na wakininenea yaliyo ndani ya mioyo yao, huku wakati wote wakitenda kwa njia tofauti kabisa pasi na ufahamu Wangu. Binadamu vipofu! Mnajua kidogo sana kabisa—Mungu ambaye huangalia kwa kina sana ndani ya moyo wa mwanadamu. Bado hamnijui Mimi hata sasa; bado mnafikiri Sijui kile unachonui. Fikiria jambo hilo: Ni watu wangapi ambao wamejiangamiza kwa sababu ya ubinadamu Wangu wa kawaida? Amka! Usinidanganye tena. Lazima uweke tabia na mwenendo wako wote, kila neno na tendo lako mbele Yangu, na ukubali ukaguzi Wangu wa hilo.

Sura ya 77

Kutokuwa na hakika ya maneno Yangu ni sawa na kushikilia mtazamo wa kukanusha kuelekea matendo Yangu. Yaani, maneno Yangu yamebubujika kutoka ndani ya Mwanangu, lakini hamyatili maanani. Ninyi hamko makini! Maneno mengi yamebubujika kutoka ndani ya Mwanangu, lakini ninyi ni wenye mashaka, hamyajui sana. Ninyi ni vipofu! Hamwelewi madhumuni ya kila kitu ambacho Nimefanya. Je, maneno Ninayoyaeleza kupitia kwa Mwanangu si maneno Yangu? Kuna mambo mengine ambayo Siko tayari kuyasema moja kwa moja, kwa hiyo Nazungumza kupitia kwa Mwana Wangu. Lakini kwa nini ninyi ni wenye upuuzi sana kiasi kwamba mnasisitiza Ninene moja kwa moja? Hunielewi Mimi, na kila mara una mashaka kuhusu vitendo na matendo Yangu! Je, Sijasema hapo awali kwamba kila hatua Yangu na kila kitendo Changu ni sahihi? Watu wanapaswa kuacha kuyachunguza. Ondoa mikono yako michafu! Hebu Nikuambie: Watu wote ambao Mimi huwatumia waliamuliwa kabla ya Mimi kuumba ulimwengu, na pia wanaidhinishwa na Mimi leo. Ninyi daima mnatia bidii kwa mambo kama hayo, mkichunguza mtu Niliye na kuyachunguza matendo Yangu. Ninyi nyote mna mawazo ya wafanyabiashara. Hili likitokea tena basi hakika mtaangushwa kwa mkono Wangu Ninachosema ni: Usinishuku, na pia usichanganue au kufikiri juu ya mambo ambayo Nimeyatenda. Aidha, usiingilie mambo kama hayo. Ni kwa sababu hii inahusiana na amri Zangu za utawala. Hili sio jambo dogo!

Tumia wakati kufanya yote Niliyoyaagiza. Hebu Niseme tena, na pia kama onyo: Wageni wako karibu kufurika nchini China. Hii ni kweli kabisa! Najua watu wengi wana mashaka juu ya jambo hili na hawana hakika, kwa hivyo Nawakumbusha tena na tena ili kwamba muweze kutafuta ukuaji wa maisha kwa haraka na kuweza kuyaridhisha mapenzi Yangu mapema iwezekanavyo. Kuanzia sasa, hali ya kimataifa itakuwa na fadhaa hata zaidi, na nchi mbalimbali zitaanza kuanguka kutoka ndani. Hakutakuwa tena na siku za furaha nchini China. Yaani, wafanyakazi watagoma, wanafunzi wataacha masomo yao, wafanyabiashara wataacha masoko, na viwanda vitafungwa vyote na havitaweza kudumu. Wale maofisa wa jeshi wataanza kuandaa fedha za kutoroka (hii, pia, itatumikia mpango Wangu wa usimamizi), na viongozi wa serikali kuu katika ngazi zote pia watakuwa na shughuli nyingi sana wakizingatia mambo fulani huku wakiacha mengine yahari bika huku wote wakifanya maandalizi (hii ni ili kutumikia hatua ifuatayo). Angalia hili vizuri! Hili ni jambo linalohusisha ulimwengu wote, si tu China, kwa maana kazi Yangu inaelekezwa kwa ulimwengu wote, lakini pia inatumika kulifanya kundi la wazaliwa wa kwanza kuwa wafalme. Je, mnaona hili waziwazi? Harakisha mtafute! Sitawatendea pasi na haki; Nitawaruhusu mpate furaha hadi mridhike.

Matendo Yangu ni ya ajabu. Wakati ambapo kuna maafa makubwa ulimwenguni, wakati

ambapo waovu wote na wakuu wanapokea adhabu—au kuwa wazi, wakati ambapo waovu walio nje ya jina Langu wanateseka—Nitaanza kuwapa baraka Zangu. Hii ndio maana halisi ya maneno “Bila shaka hamtapitia uchungu au madhara ya maafa” ambayo Nimesema mara kwa mara hapo zamani. Je, mnaelewa hili? “Wakati huu” Ninaozungumzia unahusu wakati ambapo maneno yanatokana kinywani Mwangu. Kazi ya Roho Mtakatifu ni ya haraka sana; Sitakawia au kupoteza dakika au sekunde, lakini badala yake Nitafanya kulingana na maneno Yangu mara tu yanaponenwa. Nikisema kuwa leo Ninamwondoa mtu au Namdharau mtu, yote yatakwisha kwa mtu huyo mara moja. Hiyo ni kusema kwamba Roho Mtakatifu Wangu ataondolewa mara moja kutoka kwake na atakuwa mfu anayetembea, mtu asiye na maana. Anaweza kuwa bado anapumua, kutembea na kuzungumza, na anaweza bado kuomba mbele Yangu, lakini hatawahi kutambua kwamba Nimemwacha. Yeye hasa ni mtu asiye na maana. Hii bila shaka ni kweli na halisi!

Maneno Yangu yanamwakilisha mwanadamu niliye. Kumbuka hili! Msiwe na shaka; lazima muwe na hakika kabisa. Haya ni mapambano ya kufa na kupona! Hili ni jambo zito sana! Katika wakati ambapo maneno Yangu yanazungumzwa, kile Ninachotaka kufanya kimefanyika. Lazima maneno haya yote yanenwe kupitia kwa Mwanangu. Ni nani kati yenu ametafakari jambo hili kwa uzito? Ninaweza kuelezea jambo hili vipi tena? Msiwe wenye kutishwa na waoga kila mara. Je, Mimi ni mtu Asiyewafikiria wengine? Je, Nitawatupa nje wale ambao Ninawaidhinisha bila mpango? Kila kitu Ninachofanya kina kanuni. Sitalivunja agano Nililoliweka Mimi Mwenyewe; Sitauvuruga mpango Wangu Mwenyewe. Mimi si mjinga kama ninyi. Kazi Yangu ni jambo kuu; ni kitu ambacho hakuna mwanadamu anayeweza kufanya. Nimesema kuwa Mimi ni mwenye haki, na kwamba Ninawapenda wale wanaonipenda. Je, huamini kuwa hii ni kweli? Unaendelea kuwa na shaka! Iwapo dhamiri yako iko wazi kuhusu kila kitu, basi kwa nini bado unaogopa sana? Yote ni kwa sababu umejifunga. Mwanangu! Nimekukumbusha mara nyingi usiwe na huzuni na usitoe machozi, nami Sitakutupa. Je, bado huwezi kuniamini? Mimi Nitakushikilia na Sitakuachilia. Nitakukumbatia daima katika upendo Wangu. Nitakutunza, kukulinda, na katika kila jambo kukupa ufunuo na ufahamu wa kukuwezesha kuona kwamba Mimi ni Baba yako, msaada wako. Najua kuwa daima wewe hutafakari jinsi ambavyo unaweza kupunguza mzigo ulio juu ya mabega ya Baba yako. Huu ndio mzigo Niliokupa. Usijaribu kuudharau! Ni wangapi leo wanaweza kuwa waaminifu Kwangu? Natumaini unaweza kuongeza kasi ya mafunzo yako na kukua haraka ili kuukidhi moyo Wangu. Baba humfanyia mtoto kazi kwa bidii usiku na mchana, hivyo pia lazima mwana aufikirie mpango wa usimamizi wa Baba kila dakika na kila sekunde. Huu ndio ushirikiano wa shauku pamoja na Mimi ambao Nilikuwa na mazoea ya kuuzungumzia.

Haya yote ni shughuli Yangu. Nitaweka mzigo juu ya watu Ninaowatumia leo na kuwapa

hekima, ili yale yote wanayoyatenda yatakubaliana na mapenzi Yangu, ili ufalme Wangu utimizwe, na mbingu na nchi mpya zitatokea. Watu ambao Siwatumii ni kinyume kabisa. Kila mara wao huwa wametunduwa, wao hulala baada ya kula, na hula baada ya kulala, bila kujua kabisa maana ya mzigo. Watu hawa wanakosa kazi ya Roho Mtakatifu na wanapaswa kusafishwa kutoka katika kanisa Langu haraka iwezekanavyo. Sasa Nitawasiliana kuhusu baadhi ya mambo juu ya kipengele cha maono: Kanisa ni sharti la kwanza la ufalme. Watu wanaweza tu kuingia katika ufalme mara kanisa linapojengwa kwa kiwango fulani. Hakuna mtu anayeweza kuingia katika ufalme moja kwa moja (ikiwa hakuahidiwa na Mimi). Kanisa ni hatua ya kwanza, ilhali ufalme ni kusudi la mpango Wangu wa usimamizi. Kila kitu kitakuwa katika hali nzuri watu watakapoingia katika ufalme na hakutakuwa na chochote cha kuogopa. Sasa, ni wazaliwa Wangu wa kwanza pekee na Mimi ambao tumeingia katika ufalme na tumeanza kutawala mataifa yote na watu wote. Yaani, ufalme Wangu unaanza kuwa na mpangilio, na wote ambao watakuwa wafalme au watu Wangu wametangazwa hadharani. Mtaambiwa matukio ya baadaye hatua kwa hatua na kwa utaratibu. Hupaswi kuwa na wasiwasi au wahaka sana. Je, unakumbuka kila neno ambalo Nimekumbia? Ikiwa kwa kweli uko upande Wangu, basi Nitazungumza kwako kwa uaminifu. Kwa mintarafu ya wale wanaotenda ulaghai na udanganyifu, Nitawachukulia kwa namna isiyo ya dhati pia, na kuwaacha waone vizuri kabisa ni nani atakayeangamizwa na mwenendo kama huo!

Sura ya 78

Nimesema kabla ya kuwa kazi inafanywa na Mimi, sio na mwanadamu yeyote. Kwangu, kila kitu kimetulia na kufurahi, lakini na ninyi mambo ni tofauti sana na chochote mnachofanya ni kigumu sana. Kitu chochote Ninachokubali hakika kitatimizwa na Mimi, wakati mtu yeyote Ninayemkubali atakamilishwa na Mimi. Wanadamu—msiingilie katika kazi Yangu! Chote tu mnachohitaji kujishughulisha nacho ni kufuata uongozi Wangu, kufanya kile Ninachopenda, kukataa yote ambayo Ninayachukia, mjivute kutoka kwa dhambi, na mjitupe ndani ya kumbatio Langu lenye upendo. Mimi sijisifu kwenu, wala Mimi sitii chumvi. Ukweli uko hivyo kweli. Ikiwa Nasema nitaangamiza ulimwengu, basi kufumba kufumbua, ulimwengu utageuka kuwa majivu. Nyinyi mara kwa mara huwa na wasiwasi sana na kuongezea mzigo wenu wenyewe, mkiogopa sana kwamba maneno Yangu ni matupu, kwa hivyo nyinyi mnakimbia huku na kule mkijaribu “kutafuta njia ya kutokea” kwa ajili Yangu. Kipofu! Mjinga! Hujui hata thamani yako mwenyewe na unajaribu kuwa mshauri Wangu. Je, unastahili? Jialalie vizuri kwenye kioo!

Hebu Nikwambie! Waoga lazima waadibiwe kwa ajili ya uoga wao, wakati walio waaminifu zaidi watapata baraka kwa ajili ya imani yao. Ili kuwa wazi, jambo muhimu zaidi sasa ni “imani.” Wakati baraka ambazo zitawafikia hazijafichuliwa bado, nyinyi mnahitaji kufanya

jitihada zenu zote kutumia kwa ajili Yangu kwa wakati huu. Wale wanaodaiwa kuwa “kubarikiwa” na “kuteseka na janga” hurejelea kipengele hiki. Wana Wangu! Je, maneno Yangu bado yamewekwa katika mioyo yenu? “Kwa wale wanaotumia rasilimali kwa dhati kwa ajili Yangu, hakika Nitakubariki sana.” Leo, je! Unaelewa kweli maana ambayo inakaa ndani? Mimi sizungumzi maneno matupu; kutoka sasa kuendelea hakutakuwa na kitu kilichofichwa. Hiyo ni kusema kuwa mambo yaliyofichwa katika maneno Yangu kabla sasa mtaambiwa moja kwa moja, kabisa bila ya kufichwa kokote. Zaidi ya hayo, kila neno litakuwa maana Yangu ya kweli, bila kutaja kuwa kufichua watu, matukio na mambo yote yaliyofichwa mbele Yangu kutakuwa rahisi kufanywa na hakutakuwa kugumu Kwangu. Kila kitu ninachokifanya Mimi kina kipengele cha ubinadamu Wangu wa kawaida, na pia kipengele cha uungu Wangu kamili. Je, nyinyi kweli mna ufahamu wazi wa maneno haya? Hiyo ndiyo maana Ninaendelea kurudia: Usiwe na haraka nyingi sana. Kumfichua mtu au kitu si vigumu Kwangu, na daima kuna wakati kwa ajili ya hilo. Je, sivyo? Watu wengi sana wamefunuliwa maumbo yao ya kweli mbele Yangu. Iwe ni roho wa mbweha, mbwa, au mbwa mwitu, wote hufichua maumbo yao ya kweli katika wakati maalum ambao Ninaamua, kwa sababu kila kitu Ninachofanya ni sehemu ya mpango Wangu. Kuhusu hoja hii lazima uelewe vizuri kabisa!

Je! Wewe kweli unafahamu ni nini “Wakati hauko mbali sana” unalenga? Katika siku zilizopita, daima ulifikiria kuwa ilirejelea siku Yangu, lakini ninyi nyote mmekuwa mkifasiri maneno Yangu kwa msingi wa dhana zenu. Hebu nikwambie! Mtu yeyote ambaye anafasiri vibaya maneno Yangu kuanzia sasa kuendelea bila shaka ni mpuuzi! Maneno “Wakati hauko mbali sana” ambayo nilinena yanarejelea siku zenu za kufurahia baraka, yaani, siku ambapo roho zote zenye uovu zitaangamizwa na kuondolewa kanisani Mwangu, njia zote za binadamu za kufanya mambo zitakataliwa, na zaidi ya hayo yanarejelea siku zile wakati majanga yote makubwa yatashuka. Kumbuka hili! Ni “majanga yote makubwa,” na hili usilielewe vibaya tena. Majanga Yangu makubwa yatashuka juu ya ulimwengu wote kutoka mikono Yangu kwa wakati mmoja. Wale ambao wamepata jina Langu watabarikiwa na hakika hawatavumilia mateso haya. Je! Bado unakumbuka? Je, unaelewa wazi juu ya kile Nilichosema? Wakati Ninapozungumza ndio wakati Ninaanza kufanya kazi (majanga yale makubwa huja wakati huu). Nyinyi kwa kweli hamfahamu malengo Yangu. Je, mnajua kwa nini Mimi huwawekea matakwa makali namna hiyo, bila kukuonyesha huruma yoyote hata kidogo? Pindi wakati hali ya kimataifa ni ya wasiwasi, na huku wale (wanaoidaiwa kuwa) walio mamlakani ndani ya China wanafanya maandalizi yote, ndio wakati ambapo bomu la wakati linakaribia kulipuka. Wale wanaotafuta njia ya kweli kutoka kwa mataifa yale saba watafurika nchini China kama maji kupitia njia za mafuriko, bila kujali gharama. Wengine huchaguliwa na Mimi, wengine ni wa kunitumikia Mimi, lakini hakuna mwana wa kifungua mimba kati yao. Hili ni tendo Langu! Hili lilikuwa

limefanyika wakati Niliumba ulimwengu. Ondoa dhana zako za kibinadamu. Usifikiri Mimi nazungumza maneno yasiyo na maana! Yale Ninafikiri ndiyo yale Nimeyatenda. Mpango Wangu pia ni kitu ambacho Nimekwisha kutimiza. Je! Unaelewa wazi jambo hili?

Mambo yote ya kila kitu yanatulia pamoja na mawazo Yangu na kwa mpango Wangu. Mwanangu! Nilikuchagua kwa ajili yako binafsi na zaidi ya hayo kwa sababu Ninakupenda. Yeyote anayethubutu kuasi katika mawazo, au kukuza moyo wenye wivu, atakufa kwa laana Yangu na kuchomeka. Hii inahusisha amri za utawala za ufalme Wangu kwa sababu ufalme leo tayari umeundwa. Lakini mwana Wangu, wewe inabidi uwe mwangalifu na haupaswi kuichukulia hii kama aina ya mtaji. Unapaswa kuzingatia moyo wa Baba na, kwa njia hii, kutambua juhudi za Baba zenye uangalifu. Kutokana na hili, mwana Wangu lazima aelewe ni aina gani ya mtu Ninayempenda zaidi, ni aina gani ya mtu Ninayempenda pili, ni aina gani ya mtu Ninayemchukia zaidi, na ni aina gani ya mtu Ninayemchukia. Usiendelee kuongeza shinikizo kwako mwenyewe. Tabia yoyote uliyo nayo yote ilikuwa imepangwa kabla na Mimi na ni ufunuo wa kipengele kimoja cha tabia Yangu ya uungu. Ondoa mashaka yako! Sifichi chuki kuelekea wewe. Napaswa kulisema hili jinsi gani? Je, wewe bado haufahamu? Je! Bado unazuiliwa na hofu yako? Ni nani mwaminifu, ni nani mwenye shauku, ni nani ambaye ni mwaminifu, ni nani mdanganyifu—Najua yote, kwa vile kama Nilivyosema hapo awali, Najua hali ya watakatifu kama vile kiganja cha mkono Wangu.

Katika macho Yangu, kila kitu kimekwisha kutimizwa kitambo na kufichuliwa (Mimi ni Mungu anayechunguza mioyo ya ndani ya watu. Ni kwa ajili tu ya kuwaonyesha kipengele cha ubinadamu Wangu wa kawaida, ni hayo tu), lakini kwenu nyinyi imefichwa na haijatimizwa. Hii yote ni kwa sababu nyinyi hamnijui Mimi. Yote yako katika mikono Yangu, yote yako chini ya miguu Yangu, na macho Yangu yanachunguza vitu vyote; ni nani anayeweza kuepuka hukumu Yangu? Wote walio wachafu, wale walio na vitu vya kuficha, wale wanaohukumu nyuma ya mgongo Wangu, wale ambao wana upinzani katika mioyo yao, na kadhalika—watu wote ambao hawaonekani kuwa na thamani katika macho Yangu lazima wapige magoti mbele Yangu na wajitue mzigo wao wenyewe. Labda baada ya kusikia hili, watu wengine watahamasishwa kidogo, wakati wengine hawataamini ni jambo lenye uzito kiasi hiki. Hebu niwaonye! Hebu wenye hekima waharakishe kutubu! Ikiwa wewe ni mpumbavu basi subiri tu! Angalia ni nani atakabiliwa na janga wakati ufikapo!

Mbinguni bado ni mbinguni ya awali na dunia bado ni dunia ya awali, lakini kwa mtazamo Wangu mbinguni na dunia tayari zimebadilika na sio mbinguni na dunia zilivyokuwa hapo awali. Je, mbinguni inahusu nini? Unajua? Na mbinguni ya leo inahusu nini? Je, mbinguni ya zamani ilihusu nini? Hebu niwasiliane nanyi kuhusu hili: Mbinguni ya zamani ilihusu Mungu

mliyemwamini lakini ambaye hakuna mtu aliyekuwa amemwona, na alikuwa ndiye Mungu ambaye watu walimwamini kwa uaminifu wa kweli (kwa sababu hawakuweza kumwona Yeye), ilhali mbinguni ya leo inahusu ubinadamu Wangu wa kawaida na vile vile uungu Wangu kamili, yaani, Mungu huyu mtendaji Mwenyewe. Ni Mungu yule mmoja, kwa nini basi Nasema Mimi ni mbinguni mpya? Haya yote yameelekezwa kwa dhana za mwanadamu. Dunia ya leo inahusu mahali ambapo nyinyi mko. Dunia ya zamani haikuwa na mahali moja ambapo palikuwa ni patakatifu, ilhali mahali mnakoenda leo huwekwa wakfu kama patakatifu, ambayo ndiyo sababu Nasema ni dunia mpya. “Mpya” hapa inamaanisha “takatifu.” Mbinguni na dunia mpya sasa zimefanikishwa kabisa. Je! Nyinyi mmelifahamu hili kwa wazi? Nitafichua siri zote kwenu, ukurasa kwa ukurasa. Msiwe na haraka, na hata siri nyingi zaidi zitafichuliwa kwenu!

Sura ya 79

Vipofu! Wajinga! Rundo la takataka lisilo na maana! Nyinyi hutenganisha ubinadamu Wangu wa kawaida na uungu Wangu! Je, hamfikiri kuwa hii ni dhambi dhidi Yangu? Na zaidi ni kuwa ni kitu ambacho ni vigumu kusamehe! Mungu wa vitendo anakuja miongoni mwenu leo lakini mwajua tu upande Wangu mmoja ambao ni ubinadamu Wangu wa kawaida, na hamjaona kabisa upande Wangu ambao ni wa kiungu kabisa. Je, unafikiri kuwa Sijui anayejaribu kunidanganya kisirisiri? Sikukosoi sasa, ila tu kutazama ni kiwango gani ambacho unaweza kufikia na hatima yako itakavyokuwa. Maneno Yangu yamesemwa kwa maelfu na ninyi mmetenda mambo mengi mabaya. Kwa nini ninyi hujaribu kunidanganya tena na tena? Tahadhari kuhusu kupoteza maisha yako! Iwapo utachochea hasira Yangu kwa kiwango fulani basi Sitakuonyesha huruma na Nitakufukuza. Sitatazama jinsi ulivyokuwa hapo awali, iwapo ulikuwa mwaminifu au mwenye shauku, ni kiasi gani umejishughulisha, ni kiasi gani umetoa rasilimali kwa ajili Yangu—Sitatazama mambo haya hata kidogo. Unahitaji tu kunichokoza hivi sasa na Nitakutupa katika kuzimu. Nani bado anathubutu kujaribu kunidanganya? Kumbuka hili! Kuanzia sasa Ninapokasirika, bila kujali ni nani, Nitakutokomeza mara moja ili kwamba kusiweko na taabu ya siku za baadaye na ili Nisiweze kukuona tena. Ukiniasi Nitakuadibu mara moja—Je, mtakumbuka hili? Wale ambao ni werevu watatubu mara moja.

Leo, yaani sasa, Mimi ni mwenye ghadhabu. Ninyi nyote lazima muwe waaminifu Kwangu, na kutoa nafsi yako yote kwangu. Hakuwezi kuwa na kukawia tena. Usipoyasikiza maneno Yangu Nitaunyosha mkono Wangu na kukupiga. Kutokana na hili Nitamfanya kila mtu anijue, na leo Mimi ni mwenye ghadhabu na uadhama kwa vyote (hii ni kali zaidi kuliko hukumu Yangu). Nimesema maneno mengi sana lakini ninyi hamjaonyesha hisia kabisa; je, ninyi ni wapumbavu sana? Sidhani ninyi ni wapumbavu, au siyo? Ni ibilisi wa zamani ndani yenu anayetekeleza utundu—je, mnaona hili kwa uwazi? Fanyeni hima ili kuleta mabadiliko ya

kimsingi. Leo, kazi ya Roho Mtakatifu imesonga kufikia hatua hii—Je, ninyi hamjaliona hilo? Jina Langu litaenea nyumba hadi nyumba katika mataifa yote na katika pande zote na litatangazwa kutoka kwenye vinywa vya watu wazima na watoto vilevile katika ulimwengu dunia; huu ni ukweli mtupu. Mimi ni Mungu Mwenyewe wa pekee, hata zaidi Mimi pekee ndimi nafsi ya Mungu, na Mimi, ukamilifu wa mwili, ni hata zaidi dhihirisho kamili la Mungu. Yeyote anayethubutu kutonicha, yeyote anayethubutu kunionyesha uasi katika macho yake, yeyote anayethubutu kuyasema maneno ya uasi dhidi Yangu hakika atakufa kutokana na laana Yangu na ghadhabu (kutakuwa na kulaani kwa sababu ya ghadhabu Yangu). Na yeyote anayethubutu kutokuwa mwaminifu au na upendo Kwangu, yeyote anayethubutu kujaribu kunifanyia hila hakika atakufa katika chuki Yangu. Haki Yangu, uadhama na hukumu vitadumu milele na milele. Mwanzoni, Nilikuwa mwenye upendo na rehema, lakini hii si tabia ya uungu Wangu kamili; haki, uadhama na hukumu ni tabia Yangu tu—Mungu Mwenyewe mkamilifu. Wakati wa Enzi ya Neema Nilikuwa mwenye upendo na rehema. Kwa sababu ya kazi Niliyopaswa kumaliza Nilikuwa na fadhila na rehema, lakini baadaye hakukuwa na haja ya fadhila yoyote au rehema (hakujakuwepo na yoyote tangu wakati huo). Yote ni haki, uadhama na hukumu na hii ni tabia kamili ya ubinadamu Wangu wa kawaida pamoja na uungu Wangu kamili.

Wale ambao hawanijui wataangamia katika kuzimu na wale ambao wana uhakika kunihusu wataishi milele, ili watunzwe na kulindwa ndani ya upendo Wangu. Punde Ninenapo neno moja, ulimwengu mzima na miisho ya dunia hutetemeka. Ni nani anayeweza kusikia maneno Yangu na asitetemeke kwa hofu? Nani hawezi kukuza moyo ambao unanicha? Nani hawezi kujua haki Yangu na uadhama kutokana na matendo Yangu? Na nani hawezi kuona uweza Wangu na hekima ndani ya matendo Yangu? Yeyote asiyezingatia kwa hakika atakufa. Hii ni kwa sababu wale wasiozingatia ni wale wanaonipinga na wasionijua; wao ni malaika wakuu na ndio watukutu zaidi. Jichunguzeni: Yeyote aliye mtukutu, anayejidai na mwenye majivuno hakika ni mlengwa wa chuki Yangu na ataangamia!

Sasa Natamka amri za utawala wa ufalme Wangu: Vitu vyote vimo ndani ya hukumu Yangu, vitu vyote vimo ndani ya haki Yangu, vitu vyote vimo ndani ya uadhama Wangu, na haki inatendwa kwa wote. Wale ambao husema wananiamini Mimi ilhali wananipinga mioyoni mwao, au ambao mioyo yao imeniacha watafukuzwa, lakini yote ni kwa wakati Wangu mzuri. Wale ambao huzungumza kwa kejeli kunihusu, lakini kwa njia ambayo watu hawatambui, watakufa mara moja (watafariki katika roho, mwili na nafsi). Kwa wale ambao huwadhulumu ama kuwadharau wale Ninaowapenda, ghadhabu Yangu itawahukumu mara moja. Hii ni kusema kwamba wale ambao wana mioyo ya wivu kwa wale Ninaowapenda na kufikiri kuwa Mimi si mwenye haki watakabidhiwa kwa wale ambao Ninawapenda ili kuwahukumu. Wale wote wenye tabia nzuri, wanyenyekevu (pamoja na wale ambao hawana hekima) na ambao ni watiifu kwa

dhati Kwangu watabaki wote katika ufalme Wangu. Wale ambao hawajapitia katika mafunzo, kumaanisha watu ambao ni waaminifu wanaokosa hekima na ufahamu, watakuwa na uwezo katika ufalme Wangu. Hata hivyo wao pia wamepitia ushughulikiwaji na kuvunjwa. Kwamba hawajapitia mafunzo si hakika, lakini badala yake kupitia mambo hayo Nitaonyesha kila mtu uweza Wangu na hekima Yangu. Nitawafukuza wale ambao bado wananishuku sasa, Sitaki hata mmoja wao (Ninawachukia sana wale ambao bado hunituhumu wakati kama huu). Kwa matendo ambayo Mimi hufanya katika ulimwengu wote, Nitawaonyesha watu waaminifu matendo Yangu ya kustaajabisha, papo kukuza busara zao, ufahamu na utambuzi, na Mimi mara moja Nitasababisha watu wadanganyifu kuharibiwa kwa ajili ya matendo Yangu ya kustaajabisha. Wazaliwa wote wa kwanza waliokuwa wa kwanza kulikubali jina Langu (kumaanisha wale watakatifu wasio na dosari, watu waaminifu) watakuwa wa kwanza kuingia katika ufalme na kutawala mataifa yote na watu wote pamoja na Mimi, kutawala kama wafalme katika ufalme na pamoja kuhukumu mataifa yote na watu wote (kumaanisha wazaliwa wote wa kwanza katika ufalme, na sio wengine). Wale walio katika mataifa yote na watu wote ambao wamekwisha kuhukumiwa na wametubu wataingia katika ufalme Wangu na kuwa watu Wangu, na wale ambao ni wakaidi na wasiotubu watatupwa katika shimo la kuzimu (ili waangamie milele). Hukumu katika ufalme itakuwa mara ya mwisho na itakuwa utakaso Wangu kwa kina duniani. Hakutakuwa tena na udhalimu wowote, huzuni yoyote, machozi yoyote na hata zaidi hakutakuwa na dunia. Kila kitu kitakuwa dhahirisho la Kristo, kila kitu kitakuwa ufalme wa Kristo. Utukufu ulioje! Utukufu ulioje!

Sura ya 80

Kila kitu kinahitaji mawasiliano halisi na Mimi ili kupata nuru na kuangazwa; aidha, ni kwa njia hii tu ndio roho inaweza kuwa na amani. La sivyo, haitakuwa na amani. Sasa ugonjwa mbaya zaidi kati yenu ni kutenganisha ubinadamu Wangu wa kawaida kutoka kwa uungu Wangu kamili; aidha, wengi wenu husisitiza juu ya ubinadamu Wangu wa kawaida, kama kwamba kamwe hawajui kuwa Mimi nina uungu kamili pia. Hii inanikufuru Mimi! Je, mnajua? Ugonjwa wenu ni mbaya sana kiasi kwamba msipoharakisha kuurekebisha mtauawa kwa mikono Yangu. Mbele Zangu mnatenda kwa njia moja (mkionekana kama wenye heshima; wanyenyekevu na wastahimilivu), ilhali bila Mimi kufahamu nyinyi hutenda kwa njia tofauti kabisa (wanafiki kabisa, wapotovu na msio wa kujizuia, mkifanya chochote mnachotaka kufanya, mkiunda mifarakano, mkianzisha falme za kujitegemea, mkitaka kunisaliti), ninyi ni vipofu! Fungua macho yako ambayo yametiwa mchanga na Shetani! Tazama Mimi ni nani hasa! Huna aibu! Hujui kwamba matendo Yangu ni ya ajabu! Hujui kuhusu uweza Wangu! Je, ni nani ambaye ingesemekana kwamba anamfanyia Kristo huduma lakini hajaokolewa? Hujui ni wajibu gani unaotekeleza! Kwa kweli wewe huja mbele Zangu kwa kujifanya ukionyesha uzuri wako, fidhuli

sana! Mimi nitakutimua kutoka kwa nyumba Yangu, Situmii mtu wa aina hii kwa sababu sikumwamua kabla au kumchagua.

Ninafanya kile Ninachosema, wale wanaotenda uovu hawapaswi kuogopa. Simkosei mtu yeyote. Daima Mimi hutenda kulingana na mpango Wangu, Nikitenda kulingana na haki Yangu. Kwa sababu wale wanaotenda uovu wamekuwa dhuria ya Shetani tangu uumbaji, Sikuwachagua, hii ndiyo maana ya “chui hawabadili madoa yao.” Katika mambo ambayo wanadamu hawawezi kuelewa, kila kitu kimeelezwa wazi na hakuna kitu kilichofichwa Kwangu. Labda wewe unaweza kuficha kitu kutoka kwa macho ya idadi ndogo ya watu, ukiwafanya watu wachache sana wakwamini, lakini na Mimi si rahisi sana. Mwishowe huwezi kutoroka hukumu Yangu. Mtazamo wa wanadamu ni finyu, na hata wale ambao wanaweza kuelewa sehemu ndogo ya hali ya sasa wanahesabiwa kama wana ujuzi fulani. Kwangu kila kitu kinaendelea vizuri, hakuna kitu kinachonizuia hata kidogo, kwa sababu yote yako chini ya udhibiti na utaratibu Wangu. Ni nani angeweza kuthubutu kutojisalimisha chini ya udhibiti Wangu! Nani angeweza kuthubutu kuvuruga usimamizi Wangu! Nani angeweza kuthubutu kuniasi au na asiye na upendo Kwangu! Ni nani angeweza kuthubutu kuniambia jambo ambalo si kweli, badala yake aniambie uongo mtupu! Hakuna hata mmoja wao atakayetoroka mikono Yangu yenye ghadhabu. Hata kama wewe sasa umejisalimisha, na uko tayari kuadibiwa, na kuingia shimo lisilo na mwisho, Sitakuhurumia kwa urahisi. Lazima Nikutoe kutoka katika shimo lisilo na mwisho ili uwe chini ya adhabu Yangu yenye hasira (kuchukia kwa kiwango cha juu sana), Nikiona mahali unapotorokea. Kitu ambacho Ninachukia zaidi ni kutenganisha ubinadamu Wangu wa kawaida kutoka kwa uungu Wangu kamili.

Heri wale walio waaminifu Kwangu; yaani, heri wao ambao kweli wananitambua kama Mungu Mwenyewe ambaye huchunguza kwa karibu moyo wa mwanadamu. Hakika Nitazidisha baraka zenu, Nikiwawezesha kufurahia baraka nzuri katika ufalme Wangu milele. Hii pia ni njia yenye ufanisi zaidi ya kumwaibisha Shetani. Hata hivyo, usiwe na pupa au wasiwasi sana, kuna muda uliotengwa Nami kwa ajili ya kila jambo. Ikiwa muda Wangu Nilioamua kabla bado haujafika, hata kama ni sekunde kabla, Sitatenda. Mimi hutenda kwa usahihi na kulingana na mpangilio, si kutenda bila mantiki. Kwa wanadamu Mimi sina wasiwasi, Niko thabiti kama Mlima Tai—lakini hujui kwamba Mimi ni Mwenyezi Mungu Mwenyewe? Usiwe na pupa sana, yote yako mikononi Mwangu. Yote yameandaliwa kitambo, yote yanangoja kwa hamu kunitumikia. Ulimwengu dunia wote unaonekana kuwa na vurugu kutoka nje, lakini kulingana na mtazamo Wangu ni wenye utaratibu. Kile Nilichokuandalia wewe ni kwa ajili yako tu kufurahia, unatambua hili? Msijihanikize katika usimamizi Wangu, Nitawaacha watu wote na mataifa yote yaone uweza Wangu kutoka kwa vitendo Vyangu, walibariki na kulisifu jina Langu takatifu kwa ajili ya matendo Yangu ya ajabu. Kwa sababu Nilisema kuwa hakuna chochote

Ninachofanya kisicho bila msingi, lakini kila kitu kimejazwa na hekima Yangu na nguvu Zangu, kimejazwa na haki na uadhama Wangu, na hata zaidi ghadhabu Yangu.

Wale ambao mara moja wanazinduka wanaposikia maneno Yangu hakika watapata baraka Zangu na bila shaka watapata ulinzi na utunzaji Wangu. Hawatapitia mateso ya kuadibiwa; badala yake watafurahia furaha ya familia. Je, unajua hili? Mateso ni ya milele, na furaha ni ya milele hata zaidi; yote yanapitiwa kuanzia sasa hivi. Iwapo unateseka au kuona furaha, inategemea ni mtazamo upi ulio nao unapokubali dhambi yako. Kuhusu ikiwa wewe ni mmojawapo wa waliowajaalia na wateule Wangu au la, wewe unapaswa kuwa na uhakika kuhusu hilo kulingana na kile ambacho Nimesema. Unaweza kuwapumbaza watu, lakini huwezi kunipumbaza. Wale ambao Nimewajaaliana kuwateua watabarikiwa sana kuanzia sasa; wale ambao Sijawajaalia na kuwateua Nitawaadibu vikali kuanzia sasa. Hili litakuwa thibitisho Langu kwenu. Wale ambao wamebarikiwa sasa bila shaka ni wapendwa Wangu; wale ambao wanaadibiwa, haina haja ya kusema kuwa hawajaamuliwa kabla na kuchaguliwa na Mimi. Unapaswa kuelewa hili! Yaani, kama unayopata sasa ni Mimi kukushughulikia, ikiwa ni maneno Yangu ya hukumu kali, basi wewe unachukiwa na unasinywa moyoni Mwangu na wewe utakuwa yule Nitakayemtelekeza. Ikiwa unapokea faraja Yangu na unapokea utoaji Wangu wa maisha, Ninakumiliki, wewe ni mmoja wa wapendwa Wangu. Wewe huwezi kuamua jambo hili kulingana na sura Yangu ya nje. Usiwaze zaidi kuhusu jambo hili!

Maneno Yangu yanathibitisha hali halisi ya kila mtu. Je, ninyi mnaamini kwamba Ninaendeleza tu mada zisizo na mpangilio? Kwamba Ninasema chochote Ninachotaka kusema? La hash! Katika kila neno Langu pamefichwa hekima Yangu. Yachukueni tu maneno Yangu kuwa ukweli. Baada ya muda mfupi sana, wageni ambao wanatafuta njia ya kweli wataingia. Wakati huo ninyi mtapigwa na butwaa na kila kitu kitafanyika bila ugumu wowote. Je, hamjui kuwa Mimi ndiye Mwenyezi Mungu? Kwa kusikia maneno Yangu mnayaamini kabisa, sivyo? Mimi sikosei, sembuse kukosea kusema, mnajua hili? Kwa hiyo, Nimesisitiza mara kwa mara kwamba mnapaswa kukubali mafundisho Yangu kwa haraka, ili muwaongoze na kuwachunga. Je, mnajua hili? Kupitia kwenu Nitawafanya wawe wakamilifu. Hata muhimu zaidi, kupitia kwenu Nitaonyesha ishara na maajabu Yangu tele, yaani, miongoni mwa wale wanaodharauliwa na wanadamu Nimechagua kikundi cha watu kunidhihirisha, kulitukuza jina Langu, kusimamia kila kitu kwa niaba Yangu, kutawala kama wafalme pamoja nami. Kwa hiyo, kwamba Ninawafunza sasa ni usimamizi mkubwa zaidi wa ulimwengu; hili ni jambo la kushangaza ambalo wanadamu hawawezi kutekeleza. Kwa kuwakamilisha Nitamtupa Shetani ndani ya ziwa la moto na kiberiti na ndani ya shimo lisilokuwa na mwisho, Nitalitupa kabisa joka kubwa jekundu hadi life, lisiinuke tena kamwe. Kwa hiyo, wote ambao wanatupwa katika shimo lisilokuwa na mwisho ni dhuria ya joka kubwa jekundu. Ninawachukia kwa kiwango kikubwa

sana. Nimeyasababisha haya, kwani hamwezi kuona? Wote wasio waaminifu, wote wanaotumia uhalifu na udanganyifu wamefichuliwa. Wenye kiburi, wenye majivuno, wanaojidai, wajeuri ni dhuria ya malaika mkuu na wao wafanana zaidi na Shetani—wote ni maadui Zangu wa jadi, wapinzani Wangu. Lazima Niwaadhibu mmoja mmoja ili kutuliza chuki ndani ya moyo Wangu. Nitafanya hili moja moja, Nikilitua moja moja.

Sasa, hata hivyo, ziwa la moto na kiberiti na shimo lisilo na mwisho ni nini? Katika mawazo ya wanadamu ziwa la moto na kiberiti ni jambo yakinifu, lakini wanadamu hawajui kuwa haya ni maelezo yenye makosa sana, lakini bado yana nafasi fulani katika akili za wanadamu. Ziwa la moto na kiberiti ni mkono Wangu ukigawa kuadibu kwa wanadamu. Yeyote anayetupwa katika ziwa la moto na kiberiti ameuawa kwa mkono Wangu. Nafsi, roho, na miili ya watu hawa vinateseka milele. Hii ndiyo maana ya kweli ya kile Nilichosema wakati Niliposema kuwa yote yamo mikononi Mwangu. Na shimo lisilo na mwisho linamaanisha nini? Katika dhana za mwanadamu linafikiriwa kuwa lindi kuu ambalo halina mwisho na lenye kina kirefu sana. Shimo lisilo na mwisho la kweli ni ushawishi wa Shetani. Mtu akianguka mikononi mwa Shetani, mtu huyu yuko katika shimo lisilo na mwisho; hata akipata mabawa hawezi kuruka nje. Kwa hiyo, linaitwa shimo lisilo na mwisho. Watu hawa wote watapitia kuadibu kwa milele, Nimepanga iwe hivi.

Sura ya 81

Oo, enzi hii mbaya na yenye uzinzi! Nitakumeza! Mlima Sayuni! Simama unisifu Mimi! Kwa kukamilika kwa mpango Wangu wa usimamizi, kwa kukamilika kwa kazi Yangu kuu, ni nani athubutuye kutoinuka na kufurahi! Ni nani athubutuye kutoinuka na kuruka kwa furaha bila kukoma! Atakutana na kifo chake mkononi Mwangu. Mimi hutekeleza haki kwa kila mtu, bila huruma hata kidogo au upendo wa fadhila, na bila kupendelea. Watu wote! Inukeni na mtoe sifa, na mnipeni Mimi utukufu! Utukufu wote usiokoma, kutoka milele hadi milele, upo kwa sababu Yangu na ulianzishwa na Mimi. Nani anayeweza kuthubutu kujichukulia utukufu mwenyewe? Nani anayeweza kuthubutu kuchukulia utukufu Wangu kama kitu cha kimwili? Atauawa kwa mkono Wangu! Ee, wanadamu katili! Niliwaumba na kuwakimu, na Nimewaongoza mpaka leo, ila hamjui angalau hata kidogo juu Yangu na hamnipendi Mimi kabisa. Ninawezaje kuwaonyesha huruma tena? Ninawezaje kuwaokoa? Naweza tu kuwatendea kwa ghadhabu Yangu! Nitawalipa na uharibifu, Niwalipe na kuadibu kwa milele. Hii ni haki; inaweza tu kuwa kwa njia hii.

Ufalme Wangu ni imara na thabiti; hautaanguka kamwe, lakini utakuwapo hadi milele! Wana Wangu, wana Wangu wazaliwa wa kwanza, watu Wangu watafurahia baraka pamoja nami milele na milele! Wale ambao hawaelewi mambo ya kiroho na ambao hawapokei ufunuo kutoka

kwa Roho Mtakatifu wataondolewa kutoka katika Ufalme Wangu siku moja. Hawataondoka kwa hiari yao wenyewe, lakini watalazimishwa kutoka nje na utawala wa fimbo Yangu ya chuma, na utukufu Wangu, na zaidi ya hayo, watapigwa teke na mguu Wangu. Wale ambao walipagawa na roho wabaya hapo zamani (tangu kuzaliwa) watafichuliwa sasa. Nitakufukuza nje! Je, bado unakumbuka yale ambayo Nimeyasema? Mimi—Mungu mtakatifu na Asiye na waa—Siishi katika hekalu chafu na la kuchukiza. Wale ambao walikuwa wamepagawa na roho wabaya wanajua wenyewe, na Sihitaji kufafanua. Sijakujaalia! Wewe ni Shetani mkongwe, ilhali unataka kupenya katika ufalme Wangu! Hasha! Ninakuambia! Leo Nitakueleza wazi kabisa: Wale Niliowachagua wakati wa uumbaji wa wanadamu, Nimewajaza ubora Wangu na tabia Yangu; kwa hivyo, leo ni waaminifu Kwangu pekee, wanaweza kulibeeba kanisa mzigo, na wako radhi kujitoa kwa ajili Yangu na kutoa maisha yao yote Kwangu. Wale ambao Sijawachagua kwa hivyo wamepotoshwa na Shetani kwa kiwango fulani, na hawana sifa Yangu yoyote wala tabia Yangu. Mnafikiri maneno Yangu yanapingana, lakini maneno ya “Umeamuliwa kabla na kuchaguliwa na Mimi, lakini mnakubali matokeo ya matendo yenu” yote yanamrejelea Shetani. Sasa Nitaeleza jambo moja: Leo, wale ambao wanaweza kuinuka na kuchukua mamlaka ya makanisa, kuyachunga makanisa, kuudhukuru mzigo Wangu, na kuwa na kazi maalum—hakuna hata moja wa hawa ambaye anamhudumia Kristo. Wote ni wale ambao Nimewajaalia na kuwachagua. Nawaambia hili ili msiwe na wasiwasi zaidi na kuchelewesha maendeleo ya maisha yenu. Ni wangapi wanaoweza kushinda hadhi ya mzaliwa wa kwanza? Yawezekana kuwa hiki ni kitu rahisi kama kupata diploma? Haiwezekani! Kama Singewafanya muwe watimilifu, mngekuwa mmepotoshwa kwa kiasi fulani na Shetani muda mrefu uliopita. Ndiyo maana Nimesisitiza tena na tena kwamba siku zote Nitawatunza na kuwalinda wale walio waaminifu Kwangu na kuwazuia kutokana na madhara na mateso. Wale ambao Sijawajaalia ni wale ambao wamepagawa na roho wabaya, wale ambao hawajali, wapumbavu, na waliodumaa kiroho na hawawezi kuyachunga makanisa (kumaanisha wale walio na shauku lakini hawana hakika kuhusu maono). Mnapaswa kuondolewa kwa haraka mbele Yangu, na mapema iwezekanavyo ili Nisichafuke moyo na kukasirishwa na kukuona. Ukiondoka haraka, utapokea adabu kidogo, lakini kadiri unavyozidi kuchukua muda mrefu ndivyo adabu itakavyokuwa kali zaidi. Unaelewa? Usiwe mtovu wa haya sana! Wewe ni mpotovu na asiye na simile, wa kawaida na asiyejali, pasi kujua wewe ni ovyo jinsi gani! Wewe ni kipofu!

Wale wanaoshikilia mamlaka katika ufalme Wangu wote wamechaguliwa kwa uangalifu na Mimi na wamejaribiwa tena na tena; hakuna mtu anayeweza kuwashinda. Nimewapa nguvu, kwa hiyo hawataanguka kamwe au kupotea. Wamepata idhini Yangu. Kutoka siku hii na kuendelea, wanafiki wataonyesha rangi zao za kweli, na wana uwezo wa kutenda kila aina ya mambo ya aibu, lakini hatimaye hawataweza kuutoroka mkono Wangu ambao huadibu na kumteketiza

Shetani. Hekalu Langu litakuwa takatifu na safi. Yote ni ushahidi Kwangu, udhihirisho Wangu, na utukufu kwa jina Langu. Ni makao Yangu ya milele na lengo la upendo Wangu wa milele. Mara nyingi Mimi hulipapasa kwa mkono wa Upendo, kulifariji na lugha ya upendo, kilitunza kwa macho ya upendo, na kulikumbatia ndani ya kifua cha upendo, hivyo halitaanguka katika mitego ya waovu au kudanganywa na Shetani. Leo, wale ambao hunihudumia lakini hawajaokoka watatumiwa na Mimi wakati wa mwisho. Kwa nini Ninaharakisha kuvitoa vitu hivi kutoka katika ufalme Wangu? Kwa nini lazima Niwafukuze watoke mbele Yangu? Nawachukia sana! Kwa nini Siwaokoi? Kwa nini Ninawachukia? Kwa nini lazima Niwapige wafe? Kwa nini lazima Niwaangamize? (Hakuna hata kipande chao kimoja kinachoweza kubaki mbele Yangu, ikiwa ni pamoja na majivu yao.) Kwa nini? Hata joka kuu jekundu, nyoka wa kale, na Shetani wa zamani hutafuta riziki ambayo hastahili katika ufalme Wangu! Msiwe na ndoto tena! Wote wataishia kuwa bure na watageuka kuwa majivu!

Nitaharibu enzi hii, kuibadilisha iwe ufalme Wangu, na kuishi na kufurahia na watu Ninaowapenda hadi milele. Vitu hivyo visivyo safi havifai kufikiri vinaweza kubaki katika ufalme Wangu. Unafikiri kuwa unaweza kuvua samaki katika maji meusi? Sahau ndoto kama hizo! Hujui kwamba kila kitu huchunguzwa na macho Yangu! Hujui kwamba kila kitu hupangwa na mikono Yangu! Usifikiri kuwa unaheshimiwa sana! Kila mmoja wenu lazima achukue nafasi yake inayostahili. Msijifanye kuwa wanyenyekevu (ikirejelea wale waliobarikiwa) au kutetemeka na kuwa na hofu (ikirejelea wale wanaopitia taabu). Sasa, kila mtu anapaswa kujua mwenyewe ndani ya moyo wake. Hata Nisipolitaja jina lako bado unapaswa kuwa na hakika, kwa sababu Nimeelekeza maneno Yangu kwa kila mtu. Bila kujali ikiwa wewe ni mteule Wangu au la, Maneno Yangu yanaelekezwa kwa hali zenu zote za sasa. Yaani, kama ninyi ni miongoni mwa wateule Wangu, basi Nazungumzia hali ya wale Niliowachagua kulingana na maonyesho yako; kwa mintarafu ya wale ambao sio wateule Wangu, Mimi pia nanena kulingana na hali yao. Kwa hivyo, maneno Yangu yamezungumzwa kwa uhakika. Kila mtu anapaswa kuwa na hisia nzuri ya hilo. Msijidanganye! Msiogope! Kwa sababu idadi ya watu ni ndogo, ni wachache pekee, udanganyifu hautafanikisha! Yeyote Nitakayesema ni mteule amechaguliwa na bila kujali unajifanya vizuri jinsi gani, bila sifa Yangu utashindwa. Kwa sababu Mimi hutimiza neno Langu, Sivurugi mipango Yangu bila mpango; Ninafanya chochote Ninachotaka kufanya, kwa sababu kila kitu Ninachofanya ni sahihi, Mimi ni mkuu, na Mimi ni wa pekee. Una hakika juu ya hili? Unaelewa?

Sasa, baada ya kusoma maneno Yangu, wale wanaofanya maovu na walio waovu na wadanganyifu, pia wanajitahidi kutafuta maendeleo na kufanya jitihada zao za kibinafsi. Wanataka kulipa gharama ndogo tu ili kupenya katika ufalme Wangu. Wanapaswa kuweka kando fikira kama hizo! (Watu hawa hawana matumaini kwa sababu Sijawapa fursa ya kutubu.)

Mimi hulinda lango la ufalme Wangu. Je, unaamini kwamba watu wanaweza kuingia katika ufalme Wangu kama wanavyotaka? Je, unaamini kwamba ufalme Wangu utakubali aina yoyote ya takataka? Kwamba ufalme Wangu utachukua aina yoyote ya takataka isiyofaa? Umekosea! Leo, wale walio katika ufalme ni wale walio na mamlaka ya kifalme pamoja nami; Nimewakuza kwa uangalifu. Hili si jambo linaloweza kufanikishwa tu kwa kulitaka—lazima ukubaliwe na Mimi. Na hili sio jambo ambalo hujadiliwa na mtu yeyote, bali ni kitu ambacho Mimi Mwenyewe hupanga. Chochote Ninachosema hutendeka. Siri Zangu hufichuliwa kwa wale Ninaowapenda. Wale wanaofanya maovu, yaani, wale ambao Sijawachagua, hawana haki ya kuzipokea. Hata wakizisikia, hawataelewa, kwa sababu Shetani ameyafunika macho yao na kuidhibiti mioyo yao, kuharibu maisha yao yote. Kwa nini inasemwa kwamba vitendo Vyangu ni vya kushangaza na vya busara, na kwamba Mimi huhamasisha kila kitu kwa ajili ya huduma Yangu? Nitawakabidhi wale ambao hawajajaaliwa na kuchaguliwa na Mimi kwa Shetani awaadhibu na kuwapotosha, na Sitajihusisha katika kuwaadhibu; hivi ndivyo Nilivyo mwenye hekima! Ni nani ambaye amewahi kufikiria hili? Bila jitihada yoyote asilani, kazi Yangu kuu imekamilika, sivyo?

Sura ya 82

Wote wanaogopa wanaposikia neno Langu. Wote wamejawa na hofu. Mnaogopa nini? Sitawaua! Ni kwa sababu mnahisi hatia na mnaogopa kugunduliwa. Yale unayoyafanya nyuma Yangu ni ya upuuzi na yasiyo na maana kabisa. Hili limenifanya Nikuchukie sana hivi kwamba Ninatamani sana Ngingekuwa nimewatupa wale ambao Sikuwa nimewajaalia wala kuwachagua katika shimo lisilokuwa na mwisho wavunjwe vipande vipande. Hata hivyo, Nina mpango Wangu, Nina malengo Yangu. Nitayahurumia maisha yako kwa sasa, kutokufukuza hadi baada ya huduma yako Kwangu kufika mwisho. Sitaki kuona viumbe kama hawa, wao ni aibu kwa jina Langu! Je, unajua hili? Unaelewa? Maskini usiye na thamani! Elewa hili waziwazi! Unapotumiwa ni Mimi Ninayefanya hivyo na wakati ambapo hutumiwi pia ni kwa sababu Yangu. Yote yamepangwa na Mimi, na mikononi Mwangu yote ni tiifu na ya utaratibu. Yeyote athubutuye kuondoka nje ya foleni atapigwa mara moja na mikono Yangu. Mara nyingi Mimi husema “kupigwa”; je, unafikiri kwamba Mimi hufanya hivyo kwa mikono Yangu? Sikitaji kufanya hivyo! Vitendo Vyangu si vya upumbavu kama wanadamu wanavyofikiri. Ina maana gani inaposemekana kwamba kila kitu kinaanzishwa na kukamilishwa na neno Langu? Kila kitu hukamilishwa bila Mimi hata kuinua kidole. Je, unaelewa maana halisi ya neno Langu?

Kamwe Sitamwoko a yeyote kati ya wale wanaotoa huduma Kwangu. Hawana mgawo katika ufalme Wangu Hii ni kwa sababu watu hawa wanajihusisha tu na mambo ya nje badala ya kufanya mapenzi Yangu. Ingawa Ninawatumia sasa, kwa kweli wao ni watu ambao

Ninawachukia zaidi, watu ambao Ninawakirihi zaidi. Leo, Ninampenda yeyote anayefanya mapenzi Yangu, yeyote anayeweza kuidhukuru mizigo Yangu, na yeyote anayeweza kutoa kila kitu chake kwa moyo wa kweli na uaminifu, na Nitampa nuru daima, kutomwacha aende mbali na Mimi. Mara nyingi Mimi husema, “Kwa wale wanaotumia rasilimali kwa dhati kwa ajili Yangu, hakika Nitakubariki sana.” “Bariki” ina maana gani? Je, unajua? Kuhusu kazi ya sasa ya Roho Mtakatifu, inaonyesha mizigo Ninayokupa. Wote wanaoweza kuubebea kanisa mzigo, ambao hujitolea kwa dhati kwa ajili Yangu, mzigo wao na moyo wao wa kweli ni baraka kutoka Kwangu. Aidha, ufunuo Wangu kwao pia ni baraka kutoka Kwangu. Hii ni kwa sababu wale ambao hawana mzigo sasa hawajaamuliwa kabla na kuchaguliwa na Mimi; laana Yangu tayari imeshuka juu yao. Yaani, wale ambao Nimewajaalia na kuwachagua wana mgawo katika vipengele chanya vya kile Nilichosema, huku wale ambao Sijawaamulia kabla na kuwateua wana mgawo katika vipengele hasi tu vya matamko Yangu. Kadiri maneno Yangu yanavyozidi kunenwa, ndivyo maana yake inavyozidi kueleweka; kadiri Ninavyoyasema, ndivyo yanavyokuwa wazi zaidi. Kila mmoja wa wale wadanganyifu na wenye hila ambao Sijawajaalia alilaaniwa na Mimi kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu. Kwa nini inasemekana kwamba mwaka, mwezi, siku, hata saa, dakika, na sekunde ya kuzaliwa kwenu kote kumepangwa vizuri na Mimi? Nilishaamua kitambo kabla ni wagani ambao watapata nafasi ya wazaliwa wa kwanza. Wako machoni Pangu; kwa muda mrefu wameonekana kuwa wa thamani na Mimi, na kwa muda mrefu wamekuwa na nafasi katika moyo Wangu. Kila neno Nilisemalo lina uzito na hubeba mawazo Yangu. Mwanadamu hana maana! Isipokuwa wale wachache ambao Ninawapenda walio na vyeo vya wazaliwa wa kwanza, ni kina nani wachache ambao huonyesha wema kwa mapenzi Yangu? Wana wangu wana thamani gani? Watu Wangu wana thamani gani? Hapo zamani, neno “Wana Wangu” lilikuwa jina la wazaliwa Wangu wa kwanza. Lakini wale kati ya wana Wangu na watu Wangu ambao hawana aibu yoyote walidhani kuwa lilikuwa jina la heshima waliloitwa. Msichukue wajibu wa wana Wangu wazaliwa wa kwanza bila aibu, je, unastahili hili? Leo ni wale pekee ambao wamethibitishwa ndio ambao wamewekwa katika nafasi muhimu mbele Yangu. Wamepata vyeo vya wazaliwa wa kwanza. Tayari wana mgawo wa kiti Changu cha enzi, taji Langu, utukufu Wangu, na ufalme Wangu. Kila kitu kimepangwa kwa uangalifu na Mimi. Wale wote wanaopokea vyeo vya wazaliwa wa kwanza leo wote wamepitia maumivu makubwa, mateso, na shida, kama vile waliyoyakabili katika familia zao tangu kuzaliwa, matarajio yao wenyewe, kazi, ndoa, nk. Hawa wazaliwa wa kwanza hawajashinda vyeo hivi bila kulipa gharama; badala yake, tayari wamepitia vipengele vyote vya maisha: vizuri na vibaya, milima na mabonde. Wote ambao hapo zamani waliheshimiwa sana na watu wa dunia na wanaoishi katika faraja nyumbani hawana mgawo katika wazaliwa wa kwanza. Hawastahili kuwa wana wa kwanza; wao huliletea aibu jina Langu, Siwataki kabisa. Kwa wana Wangu na watu Wangu ambao Nimewachagua, pia wana sifa nzuri duniani, lakini wako mbali sana na wazaliwa Wangu

wa kwanza. Sasa Ninawatumia watu fulani, lakini miongoni mwao wengi hawastahili kuwa watu Wangu, ni walengwa wa uharibifu wa milele; wanatumiwa kutoa huduma Kwangu kwa muda, sio kwa matumizi ya muda mrefu. Wale ambao watatumiwa kwa muda mrefu tayari wameamuliwa katika moyo Wangu. Yaani, wale ambao Mimi huwaweka katika nafasi muhimu ni wale Ninaowapenda na ambao Nilianza kuwatumia muda mrefu ulipoita. Yaani, kazi yao tayari imewekwa. Kwa mintarafu ya wale ambao Ninawachukia, katika hatua ya sasa wao wanatumika tu kwa muda. Wageni watakapokuja, wazaliwa wa kwanza watafichuliwa kwenu waziwazi wakati huo.

Leo Ninawahitaji mkue kwa haraka na kuonyesha wema kwa mzigo Wangu, mzigo huu sio mzito sana, na Nitawafanya mfanye tu kilicho chini ya uwezo wenu. Najua vimo vyenu, Najua kazi mnayoweza kufanya. Najua haya yote na Ninaelewa mambo haya. Ninatamani tu kuwa wana Wangu wajinyime wenyewe kwa hiari, kwa kweli wakipenda kile Ninachopenda, kuchukia kile Ninachokichukia, kufanya kile Ninachofanya, na kusema kile Ninachosema. Msidhibitiwe na nafasi, jiografia, wakati, au mtu yeyote. Natamani kuwa roho zenu ziwe huru kila mahali na kila mmoja wenu aweze kusimama katika nafasi ya wazaliwa wa kwanza. Ni nani anayejitoa Kwangu leo? Ni nani ambaye hutumia rasilmali kwa uaminifu kwa ajili Yangu? Nani akeshaye mchana na usiku kwa ajili Yangu? Ni nani ambaye huendesha mambo ya nyumba Yangu? Ni nani ambaye hupunguza mzigo uliopo mabegani Pangu kwa ajili Yangu? Je, sio wana Wangu? Kila kitu Ninachofanya ni ili kuwafanya kamili wana Wangu na katika huduma kwa wana Wangu, unaelewa? Yote ni kwa ajili ya wazaliwa Wangu wa kwanza na Sifanyi makosa. Usifikiri Mimi huwakadiria watu vibaya. Usifikiri kwamba Ninakuchukia. Usifikiri Situmii kikamilifu vipaji bora. Usifikiri kwamba Nimekosea katika kutokujaalia. Badala yake, hustahili hilo! Je, unajua? Sasa Nitawahakikishia mambo mengine: Kila mtu anayeisisimua ghadhabu Yangu mara nyingi, yeyote ambaye ni mlengwa wa mara kwa mara wa ukosoaji Wangu au kushughulikiwa na Mimi, hakika ni mlengwa wa chuki Yangu. Hakika atakufa, hilo halina budi. Nimesema kuwa Sitawashughulikia tena wana Wangu wazaliwa wa kwanza kwa sababu watu hawa wamepitia majaribio Yangu makubwa na wamepata idhini Yangu. Yeyote Nitakayemwangalia kwa sura ya ukali atakabiliana na hatari, je, huogopi? Wengi watakufa mara tu maneno Yangu yatakapotoka kinywani Mwangu. Hata hivyo, wengine bado wanadumisha mwili wao, ni kwamba tu roho yao imekufa. Dalili ya wazi ni kwamba hawana kazi ya Roho Mtakatifu na hawana chochote kinachowazuia. (Tayari wamepotoshwa na Shetani, kufikia kiwango fulani). Kila mwili wao unapofishwa, hilo hufanyika kwa mpango Wangu unaofaa na kwa wakati ambao Nimeeleza bayana. Kifo chao cha kiroho hakiwezi kufanya huduma bora Kwangu; Nitatumia mwili wao kuonyesha maajabu ya matendo Yangu. Kutoka kwa hili watu wataondoa mashaka, watasifu bila kukoma, hakutakuwa na mmoja ambaye hatakuwa na uchaji

Kwangu, na hakuna wowote ambao hawaniogopi. Sichukulii mambo yoyote kwa urahisi; wote husihi au kufa kwa sababu Yangu na hakuna yeyote anayeweza kuondoka hadi atakapotekeleza huduma yake Kwangu. Hata Shetani hawezi kurudi kwenye shimo lisilokuwa na mwisho hadi atimize huduma yake Kwangu. Kila hatua Ninayochukua ni thabiti na salama na iliyo na msingi thabiti. Hakuna hatua ambayo Mimi huchukua iliyo ya juujuu, hata kidogo.

Ni nani anayeweza kuthubutu kulinganishwa na mimi? Ni nani anayeweza kuthubutu kunipinga? Nitakupiga mara moja! Sitaacha dalili, na mwili wako utaondolewa kabisa; hii ni bila shaka. Nitaiweka katika vitendo mara Nisemapo na hakutakuwa na kurudi nyuma. Dunia inavunjika kila siku. Watu wanaangamia kila siku. Ufalme Wangu unapata umbo kila siku. Wana Wangu wazaliwa wa kwanza wanakua kila siku. Hasira Yangu inakua kila siku, kuadibu Kwangu kunakuwa kubaya zaidi kwa siku, na neno Langu linazidi kuwa kali kwa siku. Bado mnasubiri lugha Yangu juu yenu iwe yenye huruma, sauti Yangu iwe yenye ucheshi, fikiria tena! Inategemea ni nani Ninayemshughulikia. Kwa wale Niwapendao, sauti Yangu ni ya upole, daima inayofariji. Kweni, Naweza tu kuwa mkali na mwenye hukumu, na kuongeza juu ya hayo kuadibu na hasira. Bila kujua, hali katika kila nchi ya dunia inazidi kuwa ya fadhaa, kila siku zikivunjika, kila siku zikipata machafuko. Viongozi wa kila nchi wanatumai kushinda mamlaka mwishoni. Hawataraji hili, lakini kuadibu Kwangu tayari iko juu yao. Wanajaribu sana kushika mamlaka Yangu, lakini wanaota tu! Hata kiongozi wa Umoja wa Mataifa lazima pia aombe msamaha kutoka Kwangu. Matendo maovu aliyoyafanya ni mengi. Sasa ni wakati wa adhabu. Mimi Simhurumii kwa urahisi. Wote walio mamlakani ni lazima wavue mataji yao. Ni Mimi pekee Ninayestahili kutawala juu ya vitu vyote. Kila kitu kinanitegemea Mimi. Yote yananitegemea, bila kutaja wageni wachache. Nitawapiga mara moja wale wanaonichunguza kwa makini kwa sababu kazi Yangu tayari imefika hapa. Kila siku kuna ufunuo mpya, kila siku kuna mwanga mpya. Yote yanazidi kuwa kamili. Siku ya mwisho ya Shetani inakaribia zaidi na zaidi na kuzidi kuwa wazi zaidi kuliko hapo awali.

Sura ya 83

Hujui kwamba Mimi ni Mwenyezi Mungu; hujui kwamba mambo yote na vitu vyote viko chini ya udhibiti Wangu! Maana ya kila kitu huumbwa na kukamilishwa na Mimi ni nini? Baraka au misiba ya kila mtu hutegemea utimilifu Wangu, matendo Yangu. Mwanadamu anaweza kufanya nini? Mwanadamu anaweza kufanikisha nini kwa kufikiri? Katika enzi hii ya mwisho, katika enzi hii potovu, katika dunia hii ya giza ambayo Shetani amepotosha kwa kiwango fulani, ni wachache wagani wanaoweza kupatana na mapenzi Yangu? Ikiwa ni leo, jana, au katika siku zijazo zisizo mbali, maisha ya kila mtu huamuliwa na Mimi. Ikiwa wanapokea baraka au kupitia misiba, na kama wanapendwa au kuchukiwa na Mimi yote

yaliambiwa kabisa na Mimi kwa mkupuo mmoja. Nani kati yenu athubutuye kudai kuwa hatua zako ni za kujiamulia na kwamba majaliwa yako yako katika udhibiti wako? Ni nani athubutuye kusema hivyo? Ni nani athubutuye kuwa mwasi sana? Ni nani asiyeniogopa Mimi? Ni nani aliye mwasi Kwangu ndani yake? Ni nani anayethubutu kutenda kama anavyopenda? Nitamwadibu wakati uo huo, bila shaka sitakuwa tena na huruma kwa wanadamu au kuwaokoa. Wakati huu — yaani, wakati ambapo mmekubali jina Langu—ndiyo mara ya mwisho ambapo Nitaonyesha upole wowote kwa binadamu. Yaani, Nimechagua sehemu ya wanadamu, ambao, hata kama baraka zao sio za milele, wamefurahia neema Yangu kiasi fulani; Kwa hivyo, hata kama haijaambiwa kabla kuwa utabarikiwa milele, Sikutendei vibaya, na wewe ni bora zaidi kuliko wale ambao watapata msiba moja kwa moja.

Kwa kweli, hukumu Yangu tayari imefika kiwango cha juu, ikiingia katika eneo lisilo na kifani. Hukumu Yangu ii juu ya kila mtu, sasa ni hukumu ya ghadhabu. Hapo zamani ilikuwa hukumu adhimu, tofauti sana na sasa. Watu wa zamani hawakuanza kuhisi hofu kidogo hadi walipokutana na hukumu inayotolewa, sasa wakisikia neno moja tu wanaogopa sana; mtu hata anaogopa Mimi kufungua kinywa Changu. Lakini sauti Yangu ikitoka, Ninapoanza kuzungumza, anaogopa sana hivi kwamba hajui afanye nini, akitamani sana wakati huo kujificha katika shimo ardhi, lililofichwa katika kona lenye giza kuu zaidi. Mtu wa aina hii hawezi kuokolewa kwa sababu ana roho wabaya. Ninapohukumu joka kuu jekundu, Ibilisi, atakuwa mwenye hofu, hata ataogopa kuonwa na watu; kweli yeye ni uzao wa Shetani aliyezaliwa katika giza.

Hapo zamani mara nyingi Nilitumia maneno majaaliwa na uteuzi,” hii ina maana gani hasa? Je, Mimi hujaalia na kuchagua vipi? Kwa nini mtu asiwe mmoja wa waliojaaliwa na kuchaguliwa? Unawezaje kuelewa hili? Haya yote yanahitaji ufafanuzi wa wazi kutoka Kwangu na yote yanahitaji Mimi kunena moja kwa moja. Kama Ningefichua mambo haya ndani yenu, basi wapumbavu wangeamini kwamba ni wazo lililotolewa na Shetani! Ningekashifiwa bila haki! Sasa Nitazungumza kwa uwazi, bila kuzuia kitu chochote: Nilipoumba vitu vyote, kwanza Niliumba vifaa hivyo vya kutumiwa na wanadamu (maua, nyasi, miti, mbao, milima, mito, maziwa, nchi na bahari, kila aina ya wadudu, ndege, wanyama, wengine ni kwa ajili ya watu kula, na baadhi ni kwa ajili ya binadamu kuangalia). Aina mbalimbali za nafaka ziliumbwa kwa ajili ya wanadamu kulingana na tofauti kati ya mahali; ni baada tu ya kuumba haya yote ndipo Nilianza kuwaumba wanadamu. Kuna aina mbili za watu: Wa kwanza ni wateule Wangu na waliojaaliwa; wa pili wana tabia ya Shetani, na aina hii waliumbwa kabla ya Mimi kuiumba dunia, lakini kwa kuwa walipotoshwa kabisa na Shetani kwa hivyo Nimewatelekeza. Kisha Nikaumba aina iliyochaguliwa na kuambiwa kabla na Mimi, kila mmoja akiwa na tabia Zangu kwa kiasi tofauti; kwa hivyo, wale waliochaguliwa na Mimi leo kila mmoja ana tabia Zangu kwa kiasi tofauti. Ingawa wamepotoshwa na Shetani, bado ni Wangu; kila hatua ni sehemu ya

mpango Wangu wa usimamizi. Kwamba utawala wa uaminifu katika ufalme wote ulipangwa kabla ya wakati na Mimi; wale ambao ni wadanganyifu na wenye hila hawawezi kuwa waaminifu bila kujali lolote kwa sababu wao wamezaliwa kutoka kwa Shetani, wanamilikiwa na Shetani, daima ni watumishi wa Shetani walio chini ya amri yake, lakini yote ni kwa ajili ya kutimiza mapenzi Yangu. Nimefanya hilo liwe wazi ili kuondoa kukisia kwenu. Wale Ninaowakamilisha, Nitawatunza na kuwalinda; kwa wale Ninaowachukia, baada ya huduma yao kuisha wataondoka mahali Pangu. Watu hawa wanapotajwa Mimi hukasirika, watajwapo Ninataka sana kuwashughulikia wakati huo huo, lakini Ninajizuia katika vitendo Vyangu; Mimi ni mwenye kufikiria katika vitendo Vyangu na kauli Zangu. Naweza kuunyanyasa ulimwengu kwa hasira, lakini isipokuwa wale Niliowajaalia; baada ya kutulia Ninaweza kushikilia ulimwengu katika kiganja cha mkono Wangu, hiyo ni kusema Mimi hudhibiti kila kitu. Ninapoona kwamba ulimwengu umepotoshwa kwa kiasi ambacho watu hawawezi kuuvumilia, Nitauharibu mara moja. Je, si hilo litahitaji tu neno Langu moja?

Mimi ni Mungu wa vitendo Mwenyewe; Sifanyi ishara za ajabu na maajabu, lakini kila pahali hujaa kazi Zangu za ajabu. Njia iliyoko mbele itakuwa angavu mno. Ufunuo Wangu wa kila hatua ndio njia Ninayowaonyesha, mpango Wangu wa usimamizi. Hiyo ni kusema, baadaye ufunuo utakuwa mwingi zaidi na wazi zaidi. Hata katika Ufalme wa Milenia—katika siku za usoni za karibuni—ni lazima mwendeele kulingana na ufunuo Wangu na kwa kufuata hatua Zangu. Yote yamechukua umbo, yote yameandaliwa, waliobarikiwa wana baraka za milele zinazowasubiri; wale waliopigwa wana kuadibu kwa milele kunakowasubiri. Siri Zangu ni nyingi sana kwenu, yale ambayo Kwangu ni maneno rahisi zaidi yaweza yakawa magumu sana kwenu; kwa hiyo, Nasema zaidi na zaidi, kwa sababu ninyi huelewa kidogo sana, na mnahitaji Nieleze neno kwa neno, lakini msiwe na wasiwasi mwingi, Nitawanenea kulingana na kazi Yangu.

Sura ya 84

Kwa sababu ya ukosefu wake wa ujuzi kunihusu Mimi, mwanadamu amekatiza usimamizi Wangu na kudhoofisha mipango Yangu mara zisizohesabika, lakini hawajawahi kuweza kuzuia hatua Zangu zinazoendelea mbele. Hii ni kwa sababu Mimi ni Mungu wa hekima. Pamoja na Mimi kuna hekima isiyo na mipaka; pamoja na Mimi kuna siri isiyo na mipaka na isiyoweza kueleweka. Mwanadamu hajawahi kuweza kuielewa na kuifahamu kabisa tangu zamani za kale hadi milele. Je, hilo haliko hivyo? Sio hekima tu iliyo katika kila neno Ninalolisema, kunayo pia siri Yangu iliyofichwa. Pamoja na Mimi, yote ni siri, na kila sehemu Yangu ni siri. Nyinyi mmeona tu siri leo, ambayo ni kwamba mmeona nafsi Yangu, lakini bado hamjapata kufumbua siri hii iliyofichwa. Mwanadamu anaweza tu kuingia katika ufalme Wangu kwa kufuata uongozi

Wangu. Vinginevyo, wataangamia pamoja na ulimwengu na kuwa majivu. Mimi ndiye Mungu Mwenyewe aliye kamili, na si mwingine ila Mungu mwenyewe. Misemo ya zamani kama “udhihirisho wa Mungu” tayari imepitwa na wakati; hivyo ni vitu chakavu na vikongwe ambavyo havitumiki kwa sasa. Ni wangapi kati yenu ambao wameliona hili wazi? Je, ni wangapi kati yenu wamekuwa na uhakika na Mimi kwa kiasi hiki? Yote lazima ielezwe wazi na kuagizwa na Mimi.

Ufalme wa Shetani umeharibiwa na watu wake hivi karibuni watakuwa wamemaliza huduma yao kwa ajili Yangu. Wao watafukuzwa nje ya nyumba Yangu mmoja baada ya mwingine, ambayo ni kusema kwamba hali za kweli za wale ambao wamekuwa wakijifanya huku wakijificha katika nafasi mbalimbali hapo mbeleni zote zitaonyeshwa leo, na wote wataondolewa kutoka kwa ufalme Wangu. Nyinyi lazima mkumbuke! Kutoka leo na kuendelea, wale ambao Nawaacha, ikiwa ni pamoja na wale wa zamani, ni wale ambao wanaigiza tu, wale ambao ni bandia. Walikuwa tu wakijifanya kwa ajili Yangu, na lazima waondoke jukwaani onyesho linapoisha. Wale ambao kwa kweli ni wana Wangu watakuwa katika ufalme Wangu kirasmi kupokea upendo Wangu na kufurahia baraka ambazo tayari Nimeziandaa kwa ajili yenu. Heri wazaliwa wa kwanza! Nyinyi mnafaa kwa matumizi Yangu leo kwa kuwa mlipokea mafunzo Yangu hapo awali. Amini ya kwamba Mimi ndiye mwenyezi Mungu. Mambo ambayo watu hawawezi kuyatimiza, Naweza kuyafanya bila kikwazo, na hakuna nafasi yoyote kabisa ya kubishana. Msifikiri kwamba nyinyi hamuwezi kufanya kitu chochote na ya kwamba hamfai kuwa Wangu wazaliwa wa kwanza. Nyinyi mnastahili kikamilifu! Hii ni kwa sababu Mimi ndimi Ninayefanya na huvitimiza vitu vyote. Ni kwa nini mnajihisi sasa kuwa nyinyi ni wa kimo kama hicho? Ni kwa sababu tu wakati Wangu wa kuwatumia kweli haujafika. Vipaji vikuu haviwezi kutumika kwa makusudi yasiyo ya maana; nyinyi mnaelewa? Je, nyinyi mmefungwa tu katika China ndogo kutoka kwa ulimwengu dunia wote? Hiyo ni kusema, ninyi mtapewa watu wote katika ulimwengu dunia wote mpate kuwachunga na kuwaongoza, kwa maana nyinyi ni wazaliwa wa kwanza, na kuwaongoza ndugu ndio wajibu mnaopaswa kuutimiza. Jueni hili! Mimi ni mwenyezi Mungu! Nasisitiza mara nyingine tena kuwa Nawaruhusu kufurahia. Mimi ndiye Ninayefanya kazi—Roho Mtakatifu anafanya kazi kila mahali na binafsi anachukua uongozi.

Watu hawakuelewa wokovu Wangu hapo zamani—je, mnalielewa wazi jambo hili sasa? Wokovu Wangu unajumuisha vipengele kadhaa: Mojawapo ni kuwa hakuna majaaliwa kwa watu wengine hata kidogo, ambayo inamaanisha kuwa hawawezi kufurahia neema Yangu hata kidogo; kipengele kingine ni kwamba kuna wale ambao wamejaaliwa mwanzoni, ambao wanafurahia neema Yangu kwa kipindi cha wakati lakini ambao wataondolewa na Mimi baada ya wakati fulani, wakati ambao Nitaamua kabla, na kisha maisha yao yataisha kabisa; kipengele

kingine bado ni kwamba kuna wale ambao Nimewajaalia na kuwachagua, ambao wanafurahia baraka za milele; wanafurahia neema Yangu tangu mwanzo mpaka mwisho, ikiwa ni pamoja na taabu walizoteswa nazo kabla na baada ya Kunikubali pamoja na kupata nuru na kuangaziwa wanakopokea baada ya kunikubali Mimi. Kutoka wakati huo na kuendelea, wataanza kufurahia baraka, yaani, hao ndio Nawaokoa kikamilifu. Haya ndiyo maonyesho ya dhahiri zaidi ya kukamilika kwa kazi Yangu kuu. Ni nini, basi, ambacho baraka inarejelea? Ningependa kuuliza, Ni nini mnachotaka zaidi kukifanya? Ni nini mnachochukia zaidi? Je, ni nini mnachotumaini zaidi kukipata? Nyinyi mmepitia maumivu na taabu katika siku zilizopita yote kwa ajili ya kunipata Mimi na kwa ajili ya kukua kwa maisha yenu; hayo ni sehemu ya neema. Baraka ina maana kuwa mambo ambayo mnayachukia hayatafanyika tena kwenu wakati ujao, ambayo ni kusema, mambo haya hayatakuwako tena katika maisha yenu halisi, na yataondolewa kabisa mbele za macho yenu. Familia, kazi, mke, mume, watoto, marafiki na jamaa na hata ile milo mitatu kwa siku ambayo mnaichukia kila siku, itaondoka. (Hii inamaanisha kutozuiliwa na wakati na kutembea nje ya mwili kabisa. Mwili wako unaweza kudumishwa tu na kuridhika kwako katika roho. Ni mwili wako, sio nyama, ambao unarejelewa. Utakuwa huru kabisa na kupita kiwango cha kibinadamu. Huu ndio muujiza mkubwa zaidi na dhahiri sana ambao Mungu ameudhihirisha tangu uumbaji wa dunia). Chembe zote za mchanga zitaondolewa kutoka katika miili yenu, nanyi mtakuwa miili ya kiroho kabisa ambayo ni mitakatifu na haijatiwa doa, mkiweza kusafiri katika ulimwengu mzima na hadi miisho ya dunia. Kuanzia wakati huo kuendelea, pia mtakuwa mmeondokana na huko kuosha na kusugua, nanyi mtafurahia tu kwa ukamilifu. Kutoka wakati huo na kuendelea, nyinyi hamtashikilia tena dhana ya ndoa (kwa sababu Naifikisha mwisho enzi, sio kuumba ulimwengu), na hakutakuwa tena uchungu wa uzazi ambao ni wa mateso zaidi kwa wanawake. Wala hamtafanya kazi au kujitahidi kazini tena katika siku zijazo. Mtajizamisha kabisa katika kumbatio Langu la upendo na kufurahia baraka ambazo Nimewapa. Hili ni bila shaka. Mnapofurahia baraka hizi, neema itaendelea kuwafuata. Kile ambacho Nimewaandalia nyinyi, yaani, hazina nadra za thamani kutoka duniani kote, zote mtapewa nyinyi. Nyinyi hamuwezi kufahamu kuhusu wala hamuwezi kufikiri yote haya kwa sasa, na hakuna mwanadamu aliyefurahia hili hapo kabla. Wakati baraka hizi zitawajia, nyinyi mtajawa na furaha bila kikomo, lakini msisahau kwamba hizi zote ni nguvu Zangu, matendo Yangu, haki Yangu na hata zaidi, uadhama Wangu. (Nitawapa neema wale ambao Nitaamua kuwapa neema, na Nitawahurumia wale ambao Nitaamua kuwahurumia). Wakati huo, ninyi hamtakuwa na wazazi, wala hakutakuwa na mahusiano ya damu. Nyinyi nyote ni watu ambao Nawapenda, wana Wangu wapendwa. Hakuna mtu atakayethubutu kuwakandamiza nyinyi kutoka wakati huo na kuendelea. Utakuwa wakati wenu wa kukua na kuwa watu wazima, na wakati wenu wa kutawala mataifa kwa fimbo ya chuma! Ni nani anayethubutu kuwazuia Wana wangu wapendwa? Ni nani anayethubutu kuwashambulia wana Wangu wapendwa? Wote

watawaheshimu wana Wangu wapendwa kwa sababu Baba ametukuzwa. Vitu vyote ambavyo hakuna mtu angeweza kufikiria daima vitaonekana mbele ya macho yenu. Vitakuwa havina kikomo, wasivyoisha, visivyo na mwisho. Kabla ya muda mrefu, nyinyi hakika hamtahitaji tena kuunguzwa na jua na kuvumilia joto linalotesa. Wala hamtalazimika kuteseka na baridi, wala mvua, theluji au upepo havitawafikia. Hii ni kwa sababu Nawapenda, na yote itakuwa ni dunia ya upendo Wangu. Nitawapa kila kitu mnachotaka, nami Nitawaandaa kwa ajili ya kila kitu ambacho mnahitaji. Nani anathubutu kusema kuwa Mimi si mwenye haki? Nitakuua mara moja, kwa sababu Nimewaambia kabla ya kuwa ghadhabu Yangu (dhidi ya waovu) itaendelea milele, nami Sitaachilia hata kidogo. Hata hivyo, upendo Wangu (kwa wana Wangu wapendwa) pia utaendelea milele; Sitauzia hata kidogo.

Leo, wale wanaosikia maneno Yangu kama hukumu ni wale ambao hawako katika hali nzuri, lakini wakati wanapogundua hilo, Roho Mtakatifu huwa tayari amewaacha. Wazaliwa wa kwanza wanachaguliwa kutoka kati yenu kutoka ulimwengu dunia wote, lakini wana na watu hufanya tu sehemu ndogo miongoni mwenu. Mkazo Wangu uko katika ulimwengu dunia wote, ambao una maana kuwa wana na watu huchaguliwa kutoka mataifa yote ya dunia. Je, mnaelewa? Ni kwa nini Naendelea kusesitiza wazaliwa wa kwanza wanapaswa kukua haraka na kuwaongoza hao wageni? Je, mnaelewa maana halisi iliyo katika maneno Yangu? Hii ni kwa sababu China ni taifa ambalo Nimelilaani, limenitesa Mimi zaidi, na Nalichukia zaidi. Lazima mjue kwamba Mimi na wazaliwa Wangu wa kwanza tulikuja kutoka mbinguni na sisi ni watu wa ulimwengu. Sisi sio wa taifa lolote. Msishikilie mawazo ya kibinadamu! Hii ni kwa sababu Nimeonyesha nafsi Yangu kwenu. Kila kitu kiko juu Yangu. Je, mnaweza kukumbuka maneno Yangu? Kwa nini Nasema kuwa kuna watu wachache zaidi na zaidi miongoni mwenu na idadi ya watu imekuwa iliyosafishwa zaidi na zaidi? Hii ni kwa sababu wokovu Wangu unageuka hatua kwa hatua kuelekea katika ulimwengu dunia. Wale wanaoondolewa, ambao wamekubali jina Langu, wote ni wale ambao walihudumu kuwakamilisha wazaliwa wa kwanza. Je, mnaelewa? Kwa nini Nasema wote ni wale ambao huwahudumia wana Wangu? Sasa mmelewa kweli, sivyo? Kwa kweli idadi ni ndogo, hakika kuna wachache, lakini watu hao wamefaidika kwa kiasi kikubwa kwa sababu ya wana Wangu na wamefurahia sana neema Yangu nyingi, na hiyo ndiyo sababu Nilisema kuwa Naiokoa jamii ya wanadamu kwa mara ya mwisho. Sasa mnajua maana halisi katika maneno Yangu! Nitamwadibu sana mtu yeyote anayenipinga Mimi, nami Nitageuza uso Wangu kuelekea mtu yeyote anayenilinda Mimi, kwa sababu Nimekuwa daima, tangu mwanzo hadi mwisho, Mungu aliye adhimu na mwenye haki, na kila kitu kitafichuliwa kwenu. Nafanya kazi kwa haraka na kwa njia za ajabu, na hivi karibuni, mambo ya ajabu ambayo hayawezi kufikirika kwa wanadamu yatatokea. Nina maana kuwa mara moja na hivi karibuni, je, mnaelewa? Tafuteni kuingia katika maisha bila kuchelewa! Wana Wangu wapendwa, vitu vyote

vipo hapa kwa ajili yenu, na vitu vyote vipo kwa ajili yenu.

Sura ya 85

Mimi huwatumia watu tofauti kufanikisha mapenzi Yangu. Laana Zangu hufanikishwa kwa wale Ninaowaadibu na baraka Zangu kufanikishwa kwa wale ambao Ninawapenda. Ambao sasa hukutana na baraka Zangu na ambao hupitia laana Zangu kwa neno Langu moja na tamko Langu. Unajua kuwa yeyote yule Ninayekuwa mzuri kwake sasa ana uhakika wa kupata baraka Zangu daima (kumaanisha, kuja kunijua Mimi na kuwa na uhakika zaidi na zaidi kunihusu, wakipata mwanga na ufunuo mpya, na kuwa na uwezo wa kwenda mwendo sawa na wa kazi Yangu). Yeyote yule Nimchukiaye (hiki ni kitu kilicho ndani Yangu ambacho watu hawawezi kukiona kutoka nje) ni watu ambao kwa hakika watapitia laana Zangu, na ni wale ambao bila shaka ni miongoni mwa watoto wa joka kuu jekundu, hivyo watashiriki katika laana Yangu ya joka kuu jekundu. Kwa wale ambao Siwezi kuwatazama, ambao ubora wao una upungufu na wasioweza kukamilishwa au kutumiwa na Mimi, bado watakuwa na nafasi ya kuokolewa na watakuwa wale miongoni mwa wana Wangu. Iwapo mtu huyu hana ubora wowote Wangu, hawezi kuyaelewa mambo ya kiroho wala kunijua Mimi, lakini ana moyo ulio na shauku, basi atateuliwa kama mmoja wa watu Wangu. Ninawadhukuru wale wanaoshiriki laana Zangu kuwa wasioweza kuokolewa na ni wale ambao wamemilikiwa na roho mbaya. Nina hamu ya kuwafukuza. Wamezaliwa na joka kuu jekundu na Ninawachukia zaidi. Kuanzia sasa kuendelea Siwahitaji wao kunitolea huduma zozote—Siwataki tu! Simtaki yeyote kati yao! Hata kulia kwao na kusaga meno mbele Yangu hakuna athari—nyinyi ni vitu gani? Je, unastahili kuja mbele Yangu? Je, unastahili? Bado wanajifanya kuwa watu wazuri na kujifanya kuwa wanyenyekevu! Baada ya kuyafanya mambo mengi mno mabaya, je, Ninaweza kukuhurumia? Na kuinuka mbele Yangu unaanza kuniasi tena. Hujawahi kuwa na nia yoyote nzuri na unataka tu kunilaghai Mimi! Je, unaweza kurejea na kuwa mzuri endapo wewe ni mzao wa joka kuu jekundu? Haiwezekani! Tayari umekwisha kulaaniwa na Mimi na Ninakuhukumu kabisa! Nifanyie huduma kwa moyo wako wote, kwa uaminifu na kwa njia iliyo na nidhamu, na kisha rudi kwenye shimo la kuzimu! Je, unataka sehemu katika ufalme Wangu? Unaota! Huna aibu! Wewe uliye na mwili wenye uchafu, takataka, uliyepotoshwa sana, ilhali bado una ujasiri wa kuja mbele Yangu! Ondoka! Ukichelewa hata kidogo Nitakuadhibu vikali! Wale wote wanaojihusisha na upotovu na udanganyifu mbele Yangu lazima wafunuliwe. Je, unaweza kujificha wapi? Je, mnaweza kujisetiri wapi? Je, mnaweza kuepuka udhambi Wangu bila kujali utakwepa au kujificha kiasi gani? Usiponitolea huduma vema basi maisha yako yatakuwa mafupi hata zaidi—utamalizwa mara moja!

Ninawaambia dhahiri ni watu wa aina gani walio wazaliwa Wangu wa kwanza na

Ninawapa mathibitisho sahihi. Nisingefanya hivyo, basi msingeweza kuchukua nafasi zenu zinazowafaa na mngejiamulia wenyewe pahali ambapo panawafaa. Wengine wangukuwa wanyenyekevu zaidi na wengine wangukuwa wenye kiburi zaidi, na wale wasiomiliki ubora Wangu, au wale ambao ubora wao unakosa kabisa wote wangetaka kuwa wazaliwa Wangu wa kwanza. Je, ni maonyesho gani ambayo yanafanywa na wale ambao ni wazaliwa Wangu wa kwanza? Kwanza, wao husisitiza kuyaelewa mapenzi Yangu, wanadhukuru juu ya mapenzi Yangu na wakati huo huo wote wanashughulikiwa na Roho Mtakatifu; pili, wao huendelea kutafuta katika roho, wao si wenye kupotoka, wao huwa katika mipaka Yangu kila wakati, ni wa kawaida sana, na tabia hizo si za kuiga (kwa kuwa wanalenga kuhisi kazi ya Roho Mtakatifu na wanadhukuru juu ya upendo Wangu kwao, wao ni waangalifu katika kila wakati na wana hofu kuu ya kuwa na moyo ambao unanisali au kuniasi Mimi); tatu, wao hutenda kwa moyo wote kwa ajili Yangu, wana uwezo wa kutoa nafsi zao zote, na tayari wamekwisha kulifuta wazo lolote la matumaini yao ya baadaye, maisha yao, wanachokula, kuvaa, kutumia au wanapoishi; la nne, wao daima huwa na moyo ambao huwa na njaa na kiu ya haki, wao huamini kuwa wana upungufu mwingi na kuwa vimo vyao si pevu; la tano, ni wale ambao Nimewataja mbeleni, kuwa wale ambao wana sifa nzuri duniani lakini wametupwa kando na watu wa kidunia, na ambao wana uaminifu wa maadili katika mahusiano yao na jinsia tofauti. Haya yote ni uthibitisho, lakini sasa Siwezi kuwafunulia yote kabisa kwa kuwa kazi Yangu bado haijafikia hatua hiyo. Wazaliwa Wangu wa kwanza, kumbukeni! Hisia za maisha ndani yenu, uchaji wenu Kwangu, upendo wenu Kwangu, ufahamu wenu Kwangu, kutafuta kwa ajili Yangu, imani yenu—haya yote ni upendo Wangu kwenu na yote ni mathibitisho Ninayowapa, ili kwamba nyote kwa kweli muwe wana Wangu wapendwa na muwe kama Mimi, kula pamoja, kuishi pamoja, kufurahia baraka na Mimi katika utukufu usio na kifani!

Siwezi kumwonea huruma yeyote aliyenitesa, wale ambao hawakuwa na ufahamu juu Yangu (pamoja na kabla jina Langu kushuhudiwa), walioamini kuwa Mimi ni mwanadamu, vilevile wale walionikufuru na kunikashifu hapo zamani. Hata wakiwa na ushuhuda mkuu sana Kwangu sasa hivi, hilo halitasaidia. Kunitesa Mimi hapo mbeleni kulikuwa kunitolea huduma na bado wao ni ala Zangu kama watanitolea ushuhuda Wangu leo. Ni wale tu ambao kwa kweli wamefanywa wakamilifu na Mimi Mwenyewe wanaoweza kutumika nami, kwa kuwa Mimi ni Mungu Mwenyewe mwenye haki, na Nimetoka katika mwili na kujitenga na mahusiano yote ambayo ni ya dunia. Mimi ni Mungu Mwenyewe na watu wote, mambo yote, na vitu vyote vilivyokuwa vimenizunguka zamani vi mikononi Mwangu. Mimi sina hisia na Mimi hutenda uhaki kwa kila kitu. Mimi ni mwadilifu, Sijachafuliwa na hata chembe ya uchafu. Je, unayaelewa maana ya maneno Wangu? Je, unaweza kutimiza hili? Watu hufikiri kuwa pia Nina ubinadamu wa kawaida, familia na hisia, lakini, je, wajua kuwa umekosea kabisa? Mimi ni Mungu! Je,

mmesahau hili? Je, mmechanganyikiwa? Bado hamnifahamu!

Haki Yangu imefunuliwa kwako kikamilifu. Njia yoyote ambayo Ninamshughulikia mtu wa aina yeyote yote hufunua haki Yangu na uadhama Wangu. Kwa kuwa Mimi ni Mungu Mwenyewe ambaye huja na ghadhabu, Sitaruhusu hata mmoja ambaye alinitesa au kunitukana aponee. Je, mnaona hili kwa udhahiri, chini ya matakwa haya makali? Wale ambao Mimi huwachagua na kuwajaalia ni kama lulu adimu ama ageti na ni wachache na waliotawanyika, kwa kuwa wale watakaotawala kama wafalme kwa hakika lazima wawe wachache zaidi kuwaliko wale ambao watakuwa watu Wangu, na hili linafichua nguvu Zangu na matendo Yangu ya ajabu. Mara nyingi Mimi husema kuwa Nitawatuza, kuwapa taji na ndani Yangu kuna utukufu usiokuwa na mwisho. Je, Ninamaanisha nini kwa kusema zawadi, taji na utukufu? Katika dhana za watu, zawadi ni vitu vya mwili, kama vile chakula, mavazi au vitu vinavyoweza kutumiwa, lakini huku ni kufikiria kwao kwa zamani; si kile Ninachomaanisha ila ni ufahamu wenye upuuzi. Zawadi ni vitu vinavyopatikana sasa hivi na ni sehemu ya neema. Lakini kuna baadhi ambavyo vinahusiana na raha za mwili, na wale wanaotoa huduma kwa ajili Yangu lakini hawajaokolewa pia wanaweza kujipatia furaha ya mwili (ingawa ni vitu vya mwili ambavyo bado vinatoa huduma Kwangu). Taji si beji ya ofisi. Hiyo ni kusema, si kitu cha mwili ambacho Ninawapa kwa ajili ya furaha yenu, lakini badala yake ni jina jipya ambalo Ninawapa, na wowote wanaoweza kulifikia jina lako jipya watakuwa wale ambao wamejipatia taji, ambayo ni kupata baraka Zangu. Zawadi na taji ni sehemu ya baraka, lakini zikilinganishwa na baraka, ni chache mno, kama vile tofauti kati ya mbingu na nchi. Utukufu hauwezi hasa kufikiwa kwa dhana za watu, kwa kuwa utukufu sio vitu vya mwili, ila ni kitu ambacho wanawaza katika dhana zisizo na kadiri. Hivyo utukufu ni nini hasa? Ina maana gani kusema kuwa mtashuka kwa utukufu pamoja na Mimi? Ukamilifu Wangu—yaani, kile Nilicho na kile Nilicho nacho, huruma na wema (kwa wana Wangu), na haki, uadhama, hukumu, ghadhabu, kulaani na kuchoma (kwa watu wote)—nafsi Yangu ni uadhama. Kwa nini Ninasema kuwa Kwangu kuna utukufu bila mwisho? Ni kwa sababu Kwangu kuna hekima bila mwisho na utele usioweza kulinganishwa. Kwa hivyo, kupanda kwa utukufu na Mimi kunamaanisha kuwa tayari mmekwisha kufanywa mkamilifu na Mimi, mna kile Nilicho na kile Nilicho nacho, mnatimilizwa na Mimi, una moyo wa uchaji Kwangu na hamnipingi; mnapaswa kuelewa sasa, siyo?

Hali yenye wasiwasi ya mataifa yote ya kidunia imefika kileleni, na wote wanajitayarisha kwa kasi kutoa huduma kwa ajili Yangu na kupokea kuchoma Kwangu. Wakati ambapo ghadhabu Yangu na uchomaji vitawasili hakutakuwa na kidokezo kabla, ilhali Ninajua kile Ninachofanya na Niko dhahiri kabisa kukihusu. Mnapaswa kuwa na uhakika kuhusu maneno Yangu na lazima mfanye hima kutayarisha kila kitu, na kujitayarisha kuwachunga wale ambao huja kutafuta kutoka ughaibuni. Kumbuka hili! China—yaani, kila mtu na mahali ndani ya

Uchina—vinapitia laana Yangu; je, mnaelewa maana ya maneno Yangu?

Sura ya 86

Watu husema kuwa Mimi ni Mungu mwenye huruma na wao husema kwamba Nitaoa wokovu kwa kila kitu Nilichokiumba—mambo haya yote yanasemwa kulingana na fikira za binadamu. Kunitaja Mimi kama Mungu mwenye huruma kunaelekezewa wazaliwa Wangu wa kwanza na kuletea Kwangu wokovu kunaelekezewa wazaliwa Wangu wa kwanza na watu Wangu. Kwa sababu Mimi ni Mungu mwenye hekima, ni wazi katika mawazo Yangu ni nani Ninaowapenda na ni nani Ninaowachukia. Kwa wale Ninaowapenda, Nitawapenda daima mpaka mwisho kabisa na upendo hautabadilika kamwe. Kwa wale Ninaowachukia, moyo Wangu hauguswi hata kidogo bila kujali ni wazuri kiasi gani. Hii ni kwa sababu wao sio Wangu na hawana sifa Zangu na hawana uzima Wangu. Hiyo ni kusema, hawakuamuliwa kabla na kuchaguliwa na Mimi, kwani Mimi siwezi kukosea. Hiyo ni kusema kwamba kila Ninachofanya kinaitwa kitakatifu na chenye heshima na Sina majuto yoyote kamwe. Katika macho ya watu, Mimi ni mkatili sana; lakini hujui kwamba Mimi ni Mungu Mwenyewe mwenye haki na uadhama? Kila kitu Changu ni sahihi; wale Ninaowachukia bila shaka watapata laana Zangu na wale Ninaowapenda kwa hakika watapokea baraka Zangu. Hii ni tabia Yangu takatifu na isiyokiukwa na hakuna mwanadamu atakayeibadilisha; hili ni bila shaka!

Leo, wale ambao kwa kweli wanakubaliana na nia Zangu hakika watakamilishwa na Mimi, kwa maana kazi Yangu ni wazi na kamilifu na Siachi chochote kisicho kamili; wale Ninaowalaani watachomwa. Hivyo kwa nini watu wengi wamelaaniwa na Mimi na bado Roho Mtakatifu bado anafanya kazi Yake juu yao (hili linasemwa kuhusiana na Mimi kutoishi katika hekalu chafu)? Je, mnaelewa maana halisi ya mambo yote na vitu vyote kuhusu kutoa huduma kwa Kristo? Roho Mtakatifu hufanya kazi Yake kupitia kwa wao Ninapotumia huduma yao, lakini kwa kawaida wakati hawako katika huduma Yangu kimsingi hawajapewa nuru katika roho yao. Hata wakinitafuta, ni kwa bidii, na hii ni hila ya Shetani, kwani kwa nyakati za kawaida, hawatilii maanani kazi Yangu hata kidogo na hawahurumii kabisa mizigo Yangu. Sasa wazaliwa Wangu wa kwanza wamekua, na hivyo Ninawafukuza na kwa hiyo Roho Wangu ameondoka kutoka kila mahali, na mkazo maalum unawekwa kwa wazaliwa Wangu wa kwanza, unaelewa? Mambo yote yanabaki kwa matendo Yangu, yanabaki kwa majaaliwa Yangu, na kubaki kwa maneno yote kutoka kinywani Mwangu. Maeneo yote ambayo yamepokea baraka Zangu lazima yawe mahali ambapo Nafanya kazi, na pia mahali ambapo kazi Yangu inatekelezwa. China ni taifa ambapo Shetani anaabudiwa zaidi na hivyo Nimelilaani, na pia ni taifa ambalo limefanya mengi zaidi kunitesa. Mimi kabisa Sitafanya kazi Yangu kwa watu chini ya ushawishi wa joka kuu jekundu. Je, unaelewa maana halisi ya maneno Yangu? Hata hivyo, Wangu na watu Wangu

ni wachache. Hakika kila kitu ki mikononi Mwangu; nguvu inapaswa kulenga na juhudi zaidi zinapaswa kutumiwa kwa wale ambao Nimewachagua na kuwaamulia kabla. Hiyo ni kusema, wale ambao ni wazaliwa Wangu wa kwanza wanapaswa kutenda haraka ili kubeba mizigo iliyo juu ya mabega Yangu mapema iwezekanavyo na kuweka jitihada zote katika kazi Yangu.

Wale wanaonitumikia, sikilizeni! Mnaweza kupokea baadhi ya neema Yangu wakati mnanitumikia. Yaani, ninyi mtajua kwa wakati kuhusu kazi Yangu ya baadaye na mambo ambayo yatatokea baadaye, lakini hamtafurahia hilo kabisa. Hii ni neema Yangu. Wakati huduma Yako imekamilika, ondoka mara moja na usikawie. Wale ambao ni wazaliwa Wangu wa kwanza hawapaswi kuwa wenye kiburi, lakini mnaweza kujivunia, kwa kuwa Nimewapa baraka za milele kwenu. Wale ambao ni walengwa wa uangamizaji hampaswi kujiletea shida au kuhisi huzuni kwa ajili ya hatima yenu; ni nani aliyekufanya kuwa mzawa wa Shetani? Baada ya kufanya huduma yako kwa ajili Yangu, unaweza kurudi tena kwenye shimo lisilo na mwisho kwa sababu hutakuwa tena na matumizi Kwangu na Nitaanza kuwashughulikia na kuadibu Kwangu. Mara Ninapoanza kufanya kazi, Nitaishughulikia mpaka mwisho; matendo Yangu yatakamilishwa, na mafanikio Yangu yatadumu milele. Hili linatumika kwa wazaliwa Wangu wa kwanza, wanangu, watu Wangu, na hili linawahusu ninyi pia—Mimi kuwadibu ninyi kutakuwa kwa milele. Nimewaambia mara nyingi kabla: Waovu wanaonipinga hakika wataadibiwa na Mimi. Unaponipinga bila ukaripiaji kutoka kwa Roho Mtakatifu, tayari umelaaniwa na baada ya hapo utapigwa chini na mkono Wangu. Ukipokea nidhamu ya Roho Mtakatifu unapokuwa na mawazo mabaya kunihusu, basi umepokea baraka Yangu. Hata hivyo, lazima uwe mwangalifu daima, usiwe mzembe kamwe, na usiwe mvivu kamwe.

Sura ya 87

Lazima uharakishe hatua na ufanye kile Nataka kufanya. Hii ni kusudi Langu lenye hamu kwenu. Inawezekana kuwa kwa wakati huu bado hamjalewa maana ya maneno Yangu? Inawezekana kuwa bado hamjui kusudi Langu? Nimezungumza wazi zaidi na zaidi, na kusema mengi zaidi, lakini, je, ninyi hamjajitahidi kujaribu kuelewa maana ya maneno Yangu? Shetani, usifikiri kwamba unaweza kuharibu mpango Wangu! Wale wanaomtumikia Shetani, yaani, uzao wa Shetani (hii inahusu wale ambao wanamilikiwa na Shetani. Wale wanaomilikiwa na Shetani kwa hakika wana uhai wa Shetani, na kwa hivyo wanaitwa kuwa uzao wa Shetani) wanaomba rehema miguuni Pangu, wanalia na kusaga meno yao, lakini Siwezi kufanya kitu kama hicho cha kijinga! Ninaweza kumsamehe Shetani? Ninaweza kuleta wokovu kwa Shetani? Haiwezekani! Ninafanya kile Ninachosema na Siwezi kujuta kamwe!

Chochote Ninachosema kinakuja kutukia, si hivyo? Lakini ninyi bado kila mara hamniamini, mnashuku maneno Yangu, na kufikiri kwamba Ninawafanyia mzaha. Hiyo kwa

kweli ya dhihaka. Mimi ni Mungu Mwenyewe! Mnaelewa? Mimi ni Mungu Mwenyewe! Ikiwa Sina hekima na sina nguvu, Ninaweza tu kufanya na kusema kama inavyonipendeza? Lakini bado hamniamini. Nimesisitiza mara kwa mara kwenu, na Nimewaambia mara kwa mara. Ni kwa nini wengi wenu bado hawaamini? Kwa nini bado mna mashaka? Kwa nini mnamshikilia kabisa mawazo yenu wenyewe? Yanaweza kukuokoa? Ninatenda kile ninachosema. Nimewaambia mara nyingi: Angalieni maneno Yangu kuwa ni ya kweli na msishuku. Je, mmechukulia maneno Yangu kwa uzito? Wewe peke yako huwezi kufanya chochote, lakini huwezi kuamini katika kile Ninachotenda. Ni nini kinaweza kusemwa juu ya mtu kama huyo? Kusema wazi wazi, ni kama kwamba Sikuwahi kuwaumba kamwe, ambayo ni kusema, wewe hujahitimu katika kila hali kuwa mtumishi Wangu. Kila mtu lazima aamini maneno Yangu! Wote wanapaswa kupitia jaribio—Sitamuacha mtu yeyote kukwepa. Bila shaka, hii ni isipokuwa wale wanaoamini. Watu wanaoyaamini maneno Yangu bila shaka watapata baraka Zangu, ambayo utapewa wewe na kutimizwa ndani yako kulingana na kile unachoamini. Wana Wangu wazaliwa wa kwanza! Sasa, Ninaanza kuwapa baraka Zangu zote. Mtaanza kuvitupa vifungo vyote vinavyochukiza vya mwili kidogo na kidogo: ndoa, familia, kula, kuvaa, kulala, majanga yote ya asili (upepo, jua, mvua, dhoruba inayouma, shida ya kuanguka kwa theluji, na mambo mengine yote mnayochukia). Ninyi mtasafiri baharini, ardhini, na angani bila kuathiriwa na vizuio vya anga, wakati, au jiografia, kujifurahisha kikamilifu katika kumbatio Langu la upendo, mkiwa na wajibu juu ya kila kitu chini ya utunzaji Wangu wa upendo.

Ni nani asiyejivunia wana Wangu wazaliwa wa kwanza ambao Nimewafanya wakamilifu? Ni nani asiyelisifu jina Langu kwa ajili ya wana Wangu wazaliwa wa kwanza? Kwa nini sasa Ninataka kuwaonyesha siri nyingi sana? Mbona si katika wakati uliopita, lakini leo? Hii yenyewe pia ni siri, wewe unajua? Kwa nini Sikusema hapo nyuma kuwa China ni taifa Nilililolilaani? Na kwa nini Sikuwafichua wale wanaonitumikia? Leo Nawaambieni hili: Leo, kwa maoni Yangu, kila kitu kimetimilika—Ninasema hili kuhusu wana Wangu wazaliwa wa kwanza. (Kwa kuwa leo wana Wangu wazaliwa wa kwanza wametawala pamoja nami, sio tu kuoneka, lakini kwa kweli wanatawala pamoja nami. Kwa sasa, ni kwa yeyote ambaye Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani yake ambaye kwa hakika anatawala pamoja nami, na hii inafichuliwa sasa, sio jana, wala kesho.) Leo Ninafichua siri zangu Zangu zote katika ubinadamu wa kawaida kwa sababu wale watu ambao Nataka kuwafichua wamefichuliwa, na hii ni hekima Yangu. Kazi Yangu imeendelea hadi hatua hii: Yaani, kwa wakati huu ni lazima Nitekeleze mpango wa maagizo ya utawala Niliyoamua juu ya wakati huu. Kwa hiyo, Ninawatunukia wana Wangu wazaliwa wa kwanza, wana, watu, na watendaji huduma thibitisho linalostahili, kwa sababu Nina mamlaka na Nitahukumu na kutatawala kwa ukali. Ni nani anayethubutu kutonifanyia huduma kwa utii? Ni nani anayethubutu kunilalamikia? Ni nani anayethubutu

kusema kwamba Mimi si Mungu wa haki? Najua, asili yenu ya kipepo imefichuliwa kwa muda mrefu mbele Yangu: Kwa yeyote Ninayekuwa mwema kwake, ninyi mnamwonea wivu na mnamchukia. Hii ni asili ya Shetani kabisa! Mimi ni mwema kwa wana Wangu—je, unathubutu kusema kuwa Mimi si mwenye haki? Naweza kukufukuza kabisa. Kwa bahati nzuri wewe unanifanyia huduma na sasa sio wakati; vinginevyo, Ningekuwa nimekufukuza!

Aina ya Shetani! Acheni kuwa washenzi! Msiseme tena! Msitende tena! Kazi Yangu imeanza kufanywa kati ya wana na watu Wangu waliochaguliwa, na tayari inaenea katika mataifa yote, makundi yote, madhehebu yote, na kazi zote za maisha nje ya China. Ni kwa nini wale wanaonipa huduma kila mara huzuiwa kiroho? Ni kwa nini hawaelewi kamwe mambo ya kiroho? Ni kwa nini kila mara Roho Yangu haifanyi kazi kwa watu hawa? Kwa ujumla, Siwezi kutumia nguvu nyingi sana juu ya wale ambao Sikuwaamulia kabla au kuwagua. Mateso Yangu yote ya awali, bidii Yangu ya kazi ya ulinzi imekuwa kwa wana Wangu wazaliwa wa kwanza na sehemu ndogo ya wana na watu, na zaidi ya hayo, pia wamekuwa kwa niaba ya kukamilika kwa ufanisi wa kazi Yangu ya baadaye, ili mapenzi Yangu yasizuiliwe. Kwa sababu Mimi ni Mungu Mwenye busara Mwenyewe, Nimepanga vizuri kila hatua. Mimi sijitahidi kwa vyoyote kubaki na mtu yeyote (hii inaelekezwa kwa wale ambao hawakuchaguliwa au kuamuliwa kabla), na Sitamuangusha mtu yeyote kwa bahati (hii inaelekezwa na waliochaguliwa na kuamuliwa kabla): Hii ni amri Yangu ya utawala, ambayo hakuna mtu anayeweza kuibadilisha! Kwa wale ambao Ninawachukia, Mimi ni mkatili; kwa wale Ninaowapenda, Ninawalinda na kuwahifadhi. Kwa hiyo, Ninatenda kile Ninachosema (Ninaowachagua, wamechaguliwa; Ninaowaamulia kabla, wameamuliwa kabla; haya ni mambo Yangu ambayo Nimeyapanga kabla ya uumbaji).

Nani anaweza kubadilisha moyo Wangu? Isipokuwa Mimi kufanya kulingana na mipango Ninayofanya Nitakavyo, ni nani anathubutu kutenda kwa pupa na kutotii amri Yangu? Hizi ni amri Zangu za utawala, na ni nani anayethubutu kuondoa moja yao kutoka Kwangu? Wote lazima wawe katika amri Yangu. Watu wengine wanasema, mtu huyo ameteseka sana, na ni mwaminifu na anafikiria moyo Wangu kabisa, lakini kwa nini hakuchaguliwa? Hii pia ni amri Yangu ya utawala. Nikisema mtu anaupendeza moyo Wangu, basi mtu huyo anaupendeza moyo Wangu na ni yule Ninayempenda; Nikisema kwamba mtu ni mtoto wa Shetani, basi mtu huyo ni yule Ninayemchukia. Usimpendekeze mtu yeyote! Je, unaweza kumng'amua? Haya yote yanaamuliwa na Mimi. Mwana ni mwana daima, na Shetani ni Shetani daima, ambayo ni kusema, asili ya mwanadamu haibadiliki. Isipokuwa Mimi Niwafanye wabadilike, wote watafuata aina yao wenyewe na hawawezi kamwe kubadilika!

Ninafichua siri Zangu kwenu kazi Yangu inavyoendelea. Leo, kazi Yangu imeendelea hadi hatua gani, je, mnajua kwa kweli? Je, mtafuata kwa kweli uongozi wa Roho Wangu kufanya kile

Ninachofanya na kusema kile Ninachosema? Ni kwa nini Nasema kuwa China ni taifa ambalo Nimelilaani? Kwanza, Niliwaumba Wachina wa leo kwa sura Yangu. Hawakuwa na roho, na mwanzoni wao walipotoshwa na Shetani na hawangeweza kuokolewa. Kwa hivyo Niliwakasirikia watu hawa na nikawalaani. Ninawachukia watu hawa zaidi, na Ninakasirika wanapotajwa kwa sababu ni watoto wa joka kubwa jekundu. Kutokana na hili mtu anaweza kufikiria wakati ambapo nchi za dunia zimetwaa kwa nguvu China. Bado ni vivyo hivyo leo, na yote imekuwa laana Yangu—hukumu Yangu yenye nguvu zaidi dhidi ya joka kubwa jekundu. Hatimaye, Nikawaumba aina nyingine ya watu, ambao pamoja nao Niliwaamulia kabla wana Wangu wazaliwa wa kwanza, wana, watu, na wale wanaonifanyia huduma, kwa hivyo kile Ninachofanya leo Nilipanga kitambo kufanya. Kwa nini wale walio katika mamlaka nchini China wanatesa mara kwa mara na kuwadhulumu ninyi? Ni kwa sababu joka kubwa jekundu halifurahii laana Yangu na ananipinga. Lakini ni chini ya aina hii ya mateso na tishio hasa kwamba Mimi huwakamilisha wana Wangu wazaliwa wa kwanza kurudisha mashambulio dhidi ya joka kubwa jekundu na watoto wake. Baadaye Nitawaainisha. Baada ya kusikiliza maneno Yangu, je, mnaelewa umuhimu wa kuwaruhusu kutawala pamoja nami? Ninaposema kwamba joka kubwa jekundu limesononeshwa kabisa hadi kifo chake, pia ni wakati wana Wangu wazaliwa wa kwanza watawale pamoja nami. Mateso ya joka kubwa jekundu ya wana Wangu wazaliwa wa kwanza hutoa huduma sana Kwangu, na wakati wana Wangu wanapokua na wanaweza kusimamia masuala ya nyumba Yangu, basi watumishi waovu (watenda huduma) wataondolewa. Kwa sababu wana Wangu wazaliwa wa kwanza watakuwa wakitawala pamoja nami na watakuwa wametimiza makusudi Yangu, Nitawasukuma watenda huduma mmoja baada ya mwingine kwenye ziwa la moto na kibiriti: Kwa vyovyote vile wanapaswa kwenda! Ninafahamu kikamilifu kwamba aina ya Shetani pia anataka kufurahia baraka Zangu, na asiyetaka kurudi chini ya miliki ya Shetani; hata hivyo, Nina amri Zangu ya utawala ambazo kila mtu lazima azingatie na ambazo zinapaswa kutekelezwa, na hakuna mtu anayeachiliwa. Baadaye, Nitawaambieni amri Zangu za utawala moja baada ya nyingine, msije kukosea.

Sura ya 88

Watu hawawezi tu kuwaza kiasi ambacho mwendo Wangu umezidisha kasi: Haya ni maajabu ambayo yametokea isiyoieleweka kwa mwanadamu. Kasi Yangu imeendelea tangu uumbaji wa dunia, na kazi Yangu haijawahi kusimama. Ulimwengu wote hubadilika siku kwa siku na watu, pia, wanabadilika mara kwa mara. Hizi zote ni sehemu ya kazi Zangu, zote ni sehemu ya mipango Yangu na, aidha, zote ni za usimamizi Wangu, na hakuna binadamu anayejua au kuelewa hivi vitu. Wakati tu Mimi Mwenyewe Ninapowaambia, wakati tu Ninapowasiliana nanyi uso kwa uso, ndipo mnajua hata kiasi kidogo kabisa; vinginevyo, hakuna kabisa yeyote anayeweza kujua kuhusu mpango makini wa mpango Wangu wa usimamizi. Hii

ndiyo nguvu Yangu kuu, na aidha, haya ndiyo matendo Yangu ya ajabu. Hivi ndivyo vitu ambavyo hakuna anayeweza kuvibadilisha. Kwa hivyo, kile Ninachosema leo ndicho kinachofanyika, na hii haiwezi kubadilika tu. Dhana za binadamu hazina hata ufahamu kidogo juu Yangu—zote ni kuropoka kwa upuuzi! Usifikiri kwamba umepata ya kutosha au kwamba umeridhika! Ninakwambia hivi: Wewe bado una mbali pa kwenda! Kwa mpango Wangu wote wa usimamizi, mnajua kidogo tu, kwa hivyo lazima msikize kile Ninachosema na mfanye chochote Ninachowaambia mfanye. Tendeni kulingana na mapenzi Yangu katika kila kitu, na hakika mtapata na baraka Zangu; yeyote aaminiye anaweza kupokea, ilhali yeyote asiyeamini atakuwa na hiyo “hakuna” ambayo alidhania imetimizwa ndani yake. Hii ni haki Yangu, na, hata zaidi ni uadhama Wangu, hasira Yangu na kuadibu Kwangu. Sitamwacha yeyote aepuke na hata wazo au kitendo kimoja.

Baada ya kuyasikia maneno Yangu, watu wengi huogopa na kutetemeka, nyuso zao zikijikunja kwa wasiwasi. Je, Nimekukosea kwa kweli? Je, inawezekana kuwa kwamba wewe si mtoto wa joka kuu jekundu? Unajifanya hata kuwa mzuri! Unajifanya hata kuwa mwana Wangu mzaliwa wa kwanza! Je, unafikiri Mimi ni kipofu? Je, unafikiri Siwezi kutofautisha kati ya watu? Mimi ndiye Mungu anayechunguza mioyo ya ndani ya watu: Hili ndilo Ninalowaambia wana Wangu, na ndilo Ninalowaambia ninyi pia, watoto wa joka kuu jekundu. Ninaona kila kitu kwa wazi, bila kufanya hata kosa dogo kabisa. Ngingekosaje kujua kile Ninachokifanya? Niko wazi kabisa kuhusu kile Ninachofanya! Kwa nini Nasema kwamba Mimi ni Mungu Mwenyewe, Muumbaji wa ulimwenguni na vitu vyote? Kwa nini Nasema kwamba Mimi ndiye Mungu anayechunguza mioyo ya ndani ya watu? Ninajua vyema hali ya kila mtu. Je, mnafikiri Sijui cha kufanya au cha kusema? Hili haliwahusu. Iweni makini msiuwawe kwa mkono Wangu; mtapoteza kwa njia hiyo. Amri Zangu za utawala hazina msamaha. Je, mnaelewa? Haya yote yaliyo hapa juu ni sehemu za amri Zangu za utawala. Kuanzia siku ile Ninayowaambia kuzihusu, mkitenda dhambi zozote zaidi, kutakuwa na adhabu, kwa sababu awali hamkuelewa.

Sasa Nawatangazia rasmi amri Zangu za utawala (zinaanza kazi kuanzia siku zilipotangazwa rasmi, kutoa kuadibu tofauti kwa watu tofauti):

Natimiza ahadi Zangu, na kila kitu kiko mikononi Mwangu: Yeyote aliye na shaka hakika atauwawa. Hakuna nafasi ya huruma yoyote; wataangamizwa mara moja, hivyo kuondoa chuki kutoka moyoni Mwangu. (Kuanzia sasa inathibitika kwamba yeyote anayeuwawa lazima asiwe mshiriki wa ufalme Wangu, na lazima awe wa ukoo wa Shetani.)

Kama wazaliwa wa kwanza wa kiume, ni sharti mtunze nafasi zenu na mtimize wajibu wenu vema, na msiwe wadadisi. Ni sharti mjitolee kwa mpango Wangu wa usimamizi, na popote muendapo, ni sharti muwe na ushuhuda mzuri Kwangu na mlitukuze jina Langu. Msitende vitu

vya aibu; kuweni mfano kwa wana Wangu wote na watu Wangu. Msiwe waasherati hata kwa muda kidogo: Lazima muonekane kila mara mbele ya kila mtu mkiwa na utambulisho wa wazaliwa wa kwanza wa kiume, na msiwe watumwa; badala yake, mnapaswa kutembea kwenda mbele kwa kujiamini. Nawaomba mlitukuze jina Langu, sio kulitia aibu jina Langu. Wale ambao ni wazaliwa wa kwanza wa kiume kila mmoja wao ana kazi yake binafsi, na hawawezi kufanya kila kitu. Hili ndilo jukumu Nililowapa, na halipaswi kuepukwa. Lazima mjitolee kwa mioyo yenu yote, kwa akili zenu zote na nguvu zenu zote, kwa kutimiza kile ambacho Nimewaaminia.

Kuanzia leo kuendelea, katika Ulimwengu wote, jukumu la kuongoza wana Wangu wote na watu Wangu wote litakabidhiwa wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume walitimize, na Nitamwadibu yeyote asiyeweza kuutoa moyo wake wote na akili katika kulitimiza. Hii ni haki Yangu. Sitawasamehe au kuwabembeleza hata wazaliwa Wangu wa kiume wa kwanza.

Ikiwa kuna yeyote kati ya wana Wangu wote au kati ya watu Wangu wote anayemdhihaki na kumtusi mmoja wa wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume, Nitamwadhibu vikali, kwa sababu wana Wangu wazaliwa wa kwanza wananiwakilisha Mimi Mwenyewe; kile ambacho mtu anawafanyia, ananifanyia Mimi pia. Hii ndiyo kali zaidi kati ya amri Zangu za utawala. Nitawaruhusu wazaliwa Wangu wa kwanza, kulingana na matamanio yao, watoe haki Yangu dhidi ya yeyote kati ya wana Wangu wote na watu Wangu anayeikiuka amri hii.

Taratibu Nitamtenga yeyote anayenitazama kipuuzi na anayelenga tu chakula Changu, mavazi na usingizi anayeshughulikia tu mambo Yangu ya nje na haudhukuru mzigo Wangu, na hatilii maanani kutimiza kazi zake inavyostahili. Hili linaelekezwa kwa wote walio na masikio.

Yeyote amalizaye kunifanyia huduma lazima aondoke kwa utiifu bila vurugu yoyote. Kuwa makini, la sivyo Nitakushughulikia. (Hii ni amri ya ziada).

Wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume watachukua fimbo ya chuma kuanzia sasa na kuendelea na kuanza kutekeleza mamlaka Yangu kutawala mataifa na watu wote, kutembea kati ya mataifa na watu wote na kuzitekeleza hukumu Zangu, haki, na uadhama kati ya mataifa yote na watu. Wana Wangu wote na watu Wangu wote wataniogopa, watanipa sifa, watanishangilia, na kunitukuza bila kukoma kwa sababu mpango wangu wa usimamizi umekamilika na wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume wanaweza kutawala nami.

Hii ni sehemu ya amri Zangu za utawala; baada ya hili, Nitawaambia kuyahusu kazi inapoendelea. Kutokana na amri za utawala zilizoko hapo juu, mtaona kasi ambayo kwayo Nafanya kazi Yangu, na vile vile ni hatua ipi ambayo kazi Yangu imefika. Hili litakuwa thibitisho.

Nimeshamhukumu Shetani. Kwa sababu mapenzi Yangu hayapingwi na kwa sababu wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume wametukuzwa pamoja na Mimi, tayari Nimetumia haki Yangu na uadhama juu ya dunia na vitu vyote ambavyo ni mali ya Shetani. Sikiinui kidole wala kumsikiliza Shetani kabisa (kwa sababu hastahili hata kuzungumza na Mimi). Nazidi tu kufanya kile Ninachotaka kufanya. Kazi Yangu inaendelea kwa ulaini, hatua kwa hatua, na mapenzi Yangu hayapingwi duniani kote. Hili limemwaibisha Shetani kwa kiwango na ameangamizwa kabisa, lakini hili peke yake halijatimiza mapenzi Yangu. Naruhusu pia wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume kutekeleza amri Zangu za utawala juu ya mambo yote yaliyo ya Shetani. Kwa upande mmoja, kile Ninachomruhusu Shetani aone ni hasira Yangu kuelekea kwake; kwa upande, mwingine Namruhusu auone utukufu Wangu (kuona kwamba wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume ndio mashahidi wakubwa sana kwa udhalilishaji wa shetani). Simwadhibu Mimi mwenyewe; badala yake, bali Naruhusu wazaliwa wangu wa kwanza wa kiume kutekeleza haki Yangu na uadhama. Kwa sababu Shetani alikuwa anawanyanyasa wana Wangu, kuwatesa wana Wangu na kuwaonea wana Wangu, leo, baada ya huduma yake kuisha, Nitawaruhusu wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume waliokomaa washughulike nalo. Shetani amekuwa hana nguvu dhidi ya maangamizi. Kiharusi cha mataifa yote duniani ndio ushuhuda mzuri zaidi; watu kupigana na nchi zikiwa vitani ni onyesho la wazi kabisa la kuanguka kwa ufalme wa Shetani. Sababu iliyofanya Sikuonyesha ishara na maajabu yoyote hapo zamani ilikuwa ili kumletea Shetani fedheha na kulitukuza jina Langu hatua kwa hatua. Wakati shetani ameangamizwa kabisa Naanza kuonyesha nguvu Zangu: kile Ninachosema kinatokea, na vitu vya kuvuka mipaka ambavyo havina usawa na fikira za kibinadamu vitatimia (hivi vinarejelea baraka zinazokuja karibuni). Kwa sababu Mimi ndimi Mungu Mwenyewe wa vitendo na Sina amri, na kwa sababu Nazungumza kulingana na mabadiliko katika mpango Wangu wa usimamizi, kwa hivyo kile Nilichosema zamani si lazima kiwe cha kutumika sasa. Msishikilie mawazo yenu wenyewe! Mimi siye Mungu anayezingatia amri; Kwangu, kila kitu ni huru, cha kuvuka mipaka, na kimeachiliwa kabisa. Labda kilichosemwa jana kimepitwa na wakati leo, au huenda kikawekwa kando leo (hata hivyo, amri Zangu za utawala, kwa sababu zimetangazwa rasmi hazitabadilika kamwe). Hizi ndizo hatua katika mpango Wangu wa usimamizi. Msishikilie kanuni. Kila siku kuna mwanga mpya na kuna ufunuo mpya, na huo ndio mpango Wangu. Kila siku mwanga wangu utafichuliwa kwako na sauti Yangu itaachiliwa kwa ulimwengu dunia. Je, unaelewa? Huu ni wajibu wako, jukumu ambalo Nimekuaminia. Ni lazima usilipuuze hata kidogo. Nitawatumia mpaka mwisho watu Ninaowaidhinisha, na hili halitabadilika kamwe. Kwa sababu Mimi ni mwenyezi Mungu, Najua ni mtu wa aina gani anayepaswa kufanya kitu kipi, na vile vile ni mtu wa aina gani anaweza kufanya kitu kipi. Huu ndio uweza Wangu.

Sura ya 89

Sio rahisi kuwa sawa na makusudi Yangu kwa kila kitu unachofanya; sio jambo la kujilazimisha kudanganya, lakini inategemea ikiwa Nilikujalia na akili Yangu kabla ya kuumbwa kwa dunia, ambalo lilikuwa jukumu Langu. Hiki sio kitu watu wanachoweza kufanya. Ninampenda yeyote ninayetaka kumpenda, na yeyote Ninayesema ni mzaliwa wa kwanza hakika ni mzaliwa wa kwanza, hii ni sawa kabisa. Unaweza kutaka kudanganya, lakini huku kutakuwa bure tu! Unadhani Sikutambui? Je, kuwa na tabia nzuri mbele Yangu inatosha? Je, ni rahisi hivyo? La hasha. Lazima uwe na ahadi Yangu, majaliwa Yangu. Je, unafikiri sijui unachokifanya nyuma Yangu? Umepotoshwa! Rudi haraka kwenye ziwa la moto na moto wa jehanamu mara tu utumishi wako Kwangu utakapoisha! Nimechukizwa, Ninajazwa na chuki kwa kukuona. Wote wanaonitumikia ambao hawatumii raslimali zao kwa uaminifu kwa ajili Yangu, ni wapotovu na wasiozuiwa, na hawatambui makusudi Yangu, baada ya utumishi wako kuisha, ondoka mbele ya macho Yangu! La sivyo Nitakutupa nje! Watu hawa hawawezi kuishi kwenye nyumba Yangu (kwa jina, kanisa) kwa muda zaidi. Lazima waondoke hapa ili kuzuia kutia jina Langu aibu, kuharibu sifa Yangu. Watu hawa wote ni wa ukoo wa joka kuu jekundu, wametumwa na joka kuu jekundu kuvuruga usimamizi Wangu. Wamebobeza katika udanganyifu kuvuruga kazi Yangu. Mwanangu! Ni lazima muone hili! Msishirikiane na watu hawa. Unapowaona watu wa aina hii nenda mbali nao kwa haraka ili kuzuia kutiwa kwenye mtego na hao na kuleta madhara katika maisha yako! Ninawachukia zaidi watu ambao huongea ovyo ovyo, wanaotenda bila kufikiria, wanaokuwa na mzaha tu na kucheka, wanaojihusisha na mazungumzo yasiyofaa. Siwataki watu hawa, wote ni wa namna ya Shetani! Kuchokoza bila sababu kabisa, je, hao ni nini? Kuongea na kufanya upuuzi, je, bado hawaoni aibu? Kwa uhalisi, mtu wa aina hii anachukuliwa kuwa wa thamani ya chini zaidi, kwa muda mrefu Nimewatazama, kwa muda mrefu Nimewatelekeza. La sivyo, kwa nini wanaongea upuuzi mara kwa mara bila ya Mimi kuwaadhibu? Wao kweli ni wa ukoo wa joka kuu jekundu! Sasa Nimeanza kuvitoa vitu hivi kimoja baada ya kingine. Je, Naweza kuwatumia wazaliwa wa Shetani kama wazaliwa Wangu wa kwanza wa kiume, kama wana Wangu na watu Wangu? Basi Sitakuwa nimechanganyikiwa? Hakika Sitafanya hivyo. Je, mnaelewa hili wazi?

Kila kitu mnachokumbana nacho leo, kiwe kizuri au kibaya, vyote vimepangwa kwa mikono Yangu yenye hekima: vyote vimepangwa, vimedhibitiwa na Mimi. Hakika hiki sio kitu ambacho mwanadamu anaweza kuwa tayari kukifanya. Watu wengine bado wanatokwa jasho kwenye viganja vyao, wakiwa na wasiwasi kunihusu; kweli hawafai kuwa na wasiwasi! Wanaisahau kazi yao kuu, kutoingia katika roho ilhali wanataka kukua katika maisha; wanatumaini bure! Hawana wasiwasi kabisa, lakini bado wanataka kuridhisha makusudi Yangu! Una wasiwasi kwa niaba Yangu, lakini Mimi sina wasiwasi. Je, una wasiwasi ya nini? Una uzembe katika kazi yako Kwangu, huku ukidanganya wazi wazi. Ninakwambia! Nitamwondoa

mtu wa aina hii kutoka kwenye nyumba Yangu kuanzia sasa. Hafai kunitumikia katika nyumba Yangu. Namchukia mtu wa aina hii kwa sababu ananikufuru kwa matendo yake. Iliposemekana “kukufuru dhidi Yangu ni dhambi isiyosameheka,” hii ilikuwa inamuashiria nani? Je, mnaelewa hili? Mtu wa aina hii anaamini kwamba hiyo shida bado haijawa mbaya sana ingawa ameshatenda dhambi. Kweli mtu huyu aliyechanganyikiwa ni kipofu, mjinga, na roho yake imetiwa kizuizi! Nitakutupa nje! (kwa sababu hili ni jaribu la Shetani Kwangu, Ninalichukia kiasi hiki na jambo hili limetajwa mara kwa mara, kila wakati linanikasirisha. Siwezi kuizuia, hakuna anayeweza kuisimamisha. Isingekuwa ni suala la wakati bado haujafika, Ngingekuwa nimeshughulikia kitambo.) (Hii ni kuhusu ukweli kwamba kwa wakati huu kuna watu wengi ambao bado hawaamini kwamba wageni watatafuta kuijaza Uchina; hata sasa bado hawaamini, kuifanya hasira Yangu kuvurugika na kuchemka.)

Ni mtu wa aina gani anayeupendeza moyo Wangu nyumbani Mwangu? Huku ni kusema, kabla ya uumbaji ni aina gani ya watu Niliowajalia waishi milele katika nyumba Yangu? Je, mnajua? Je, mmefikiria ni aina gani ya watu Ninaopenda na aina gani ya watu Ninaowachukia? Nyumba Yangu ni ya watu walio na mawazo sawa na Mimi, wanaoshiriki nyakati nzuri na ngumu pamoja nami, huku ni kusema, watu wanaoshiriki katika baraka na magumu. Hawa watu wote wanaweza kupenda Ninachopenda na kuchukia Ninachochukia. Wanaweza kukiacha kile Ninachochukia. Nikisema hawataweza kula, wako tayari kushinda njaa ili kuridhisha makusudi Yangu. Mtu wa aina hii yuko tayari kusalia mwaminifu Kwangu na kujitumia kwa ajili Yangu, wanaweza kufikiria kuhusu jitihada Zangu za bidii, daima wakinifanyia kazi kwa bidii. Kwa hivyo, kwa mtu wa aina hii, Ninampa cheo cha mzaliwa wa kwanza, Nikimpa kila kitu Nilicho nacho: Nina uwezo wa kuongoza makanisa yote, hili Ninawapa; Nina hekima, hii pia Ninawapa; Ninaweza kuteseka kwa kutenda ukweli, na pia Nitawapa watu hawa nia, kuwafanya wawe na uwezo wa kuteseka kwa kila kitu kwa ajili Yangu; Nina ubora mzuri wa tabia na hii pia Nitawapa, kuwafanya kuwa kama Mimi kabisa, bila tofauti hata kidogo, ili kwamba wengine wataniona watakapowaona watu hawa. Sasa, Nauweka uungu Wangu wote ndani ya watu hawa kuwawezesha kuishi kulingana na kipengele kimoja cha uungu Wangu kamili, kuwa ufunuo Wangu kamili; hili ndilo kusudi Langu. Usitafute kuwa kama Mimi kwa vitu vya nje (kula kama Mimi, kuvaa nguo sawa na kama Mimi), haya yote hayana maana, na mtajiangamiza tu mkivitafuta vitu hivi. Hii ni kwa sababu wale wanaotafuta kuniiga kwa nje ni kikaragosi wa Shetani, na bidii hii ni mbinu ya Shetani, ni lengo la Shetani. Unatafuta kuwa sawa na Mimi lakini unastahili? Nitakukanyaga mpaka ufe! Kazi Yangu inaendelea daima, ikienea kwa kila taifa duniani. Zifuate hatua Zangu kwa haraka!

Sura ya 90

Wote walio vipofu lazima waondoke kutoka Kwangu na wasiwepo kwa muda zaidi hata kidogo, kwani wale ambao Nataka ni wale ambao wanaweza kunijua, wanaoweza kuniona na wanaoweza kupata vitu vyote kutoka Kwangu. Na wanaoweza kweli kupata vitu vyote kutoka Kwangu ni nani? Hakika kuna wachache sana wa mtu wa aina hii na hakika watapata baraka Zangu. Nawapenda watu hawa na Nitawachukua mmoja baada ya mwingine kuwa wasaidizi Wangu wakuu, kuwa maonyesho Yangu, na Nitayafanya mataifa yote na watu wote wanisifu bila kukoma, wakishangilia bila kukoma kwa sababu ya watu hawa. Ee, Mlima Sayuni! Inua bango la ushindi na unishangilie! Kwa maana Mimi naenda ulimwenguni kote na hadi miisho ya dunia, Nikienda katika kila kona ya milima, mito na vitu vyote, kisha kurudi hapa tena. Narudi kwa ushindi na haki, hukumu, ghadhabu na kuchoma, na hata zaidi na wazaliwa Wangu wa kwanza. Mambo yote ambayo Nachukia kabisa na watu wote, masuala, na vitu ambavyo Mimi huchukia sana Natupa mbali sana. Mimi ni mshindi na Nimekamilisha yote ambayo Nataka kufanya. Nani anayethubutu kusema Sijakamilisha kazi Yangu? Nani anayethubutu kusema Sijawapata wazaliwa Wangu wa kwanza? Nani anayethubutu kusema kwamba Sijarudi kwa ushindi? Bila shaka wao ni aina ya Shetani, na ni wale wanaoona vigumu kupata msamaha Wangu. Wao ni vipofu, wao ni pepo wabaya na Ninawachukia zaidi. Katika vitu hivi Nitaanza kufichua ghadhabu yangu na ukamilifu wa hukumu Yangu, na, kwa njia ya moto Wangu unaowaka, kuwasha moto ulimwengu na dunia kutoka mwisho mmoja hadi mwingine, Nikipa nuru kila pembe—hii ni amri Yangu ya utawala.

Mara tu mnapoelewa maneno Yangu, mnapaswa kupata faraja kutoka kwayo; hampaswi kuyaacha yapite bila kuyasikiza. Matamshi ya hukumu yanakuja kila siku, kwa hiyo mbona ninyi ni wapumbavu na msiojali hivyo? Mbona hamshirikiani na Mimi? Je, mko tayari sana kwenda kuzimu? Nasema Mimi ni Mungu wa huruma kwa wazaliwa Wangu wa kwanza, wanangu na watu Wangu, hivyo mnalielewaje hili? Hii si kauli rahisi, na inapaswa kueleweka kutoka kwa mtazamo mzuri. Ee, binadamu kipofu! Nimewaokoa mara nyingi, Nikiwaleta kutoka kwa mfumbato wa Shetani na kutoka kwa kuadibu ili muweze kupata ahadi Yangu, hivyo kwa nini msionyeshe huruma kwa moyo Wangu? Je, yeyote kati yenu anaweza kuokolewa kwa njia hii? Haki Yangu, uadhama na hukumu havionyeshi huruma kwa Shetani. Lakini kwa ajili yenu, vipo ili kuwaokoa, lakini ninyi hamwezi tu kuielewa tabia Yangu, wala hamjui kanuni za matendo Yangu. Mlifikiri kuwa Natenda bila kujua ukali wa vitendo Vyangu, au kujua malengo yao—wapumbavu mlioje! Naweza kuona wazi watu wote, matukio, na vitu. Naelewa kwa uwazi kamili kiini cha kila mtu, ambayo ni kusema, Nang’amua kabisa mambo ambayo mtu anaweza ndani yake mwenyewe. Naweza kuona wazi kama mtu ni Yezebeli au mzinzi, na Najua ni nani anayefanya nini kwa siri. Usikoge hirizi zako mbele Yangu—wewe fidhuli! Ondoka hapa sasa hivi! Ili kuepuka kuliletea aibu jina Langu, Simhitaji mtu wa aina hiyo! Hawezi kulishuhudia

jina Langu, lakini badala yake anatenda kinyume na maendeleo na analeta aibu kwa familia Yangu! Atafukuzwa kutoka katika nyumba Yangu mara moja. Simtaki yeye. Sitastahimili kuchelewa kwa hata sekunde moja! Kwa watu hao ni bure bila kujali jinsi wanavyotafuta, kwa maana katika ufalme Wangu wote ni watakatifu na wasio na dosari yoyote. Ikiwa ni pamoja na watu Wangu, Nikisema kuwa Simtaki mtu fulani basi Namaanisha hilo; usisubiri Nibadili mawazo Yangu. Sijali jinsi ulivyokuwa mzuri Kwangu awali!

Ninawafichulia siri kila siku. Je, mnajua njia Yangu ya kuzungumza? Ninafichua siri zangu kwa mujibu wa nini? Je, mnajua? Mara nyingi ninyi husema kuwa Mimi ni Mungu anayewapa kwa wakati unaofaa, kwa hivyo mnaelewa vipi vipengele hivi? Ninafichua mafumbo Yangu kwenu moja baada ya lingine kulingana na hatua za Kazi Yangu, na Ninawaruzuku kulingana na mpango Wangu, na hata zaidi kulingana na vimo vyenu vya kweli (kuruzuku kunatajwa kwa kurejelea kila mtu katika ufalme). Mbinu Yangu ya kuzungumza ni hivi: Kwa watu walio nyumbani Mwangu Nawapa faraja, Nawaruzuku na Ninawahukumu; kwa Shetani Sionyeshi huruma, na yote ni hasira na kuchomeka. Nitatumia amri Zangu za utawala ili kuwatoa nje ya nyumba Yangu mmoja baada ya mwingine wale ambao Sijawaamulia kabla au kuwachagua. Hakuna haja ya kuhisi wasiwasi. Baada ya kuwafanya wafichue maumbo yao ya asili (baada ya wao kutoa huduma kwa wanangu mwishowe), watarudi kwenye shimo lisilo na mwisho, la sivyo Sitawahi kulipumzisha jambo hili na Sitaliacha kamwe. Mara nyingi watu hutaja kuzimu na jahanamu. Lakini maneno haya mawili yanarejelea nini, na tofauti kati yao ni ipi? Je, kweli yanarejelea pembe fulani ya baridi, ya giza? Akili ya binadamu daima inakatiza usimamizi Wangu, wakifikiria kwamba kutafakari kwao kusio na mpango maalumu ni kuzuri sana. Lakini haya yote ni mawazo yao wenyewe. Kuzimu na jahanamu zote zinarejelea hekalu la uchafu ambalo limeishiwa na Shetani awali au na roho wabaya. Hiyo ni kusema, yeyote ambaye amemilikiwa na Shetani au roho wabaya awali, ni wao ambao ni Kuzimu na wao ndio jahanamu—hakuna kosa kuhusu hilo! Hii ndiyo sababu Nimesisitiza kwa kurudia katika siku za nyuma kwamba Siishi katika hekalu la uchafu. Je, Mimi (Mungu Mwenyewe) Ninaweza kuishi Kuzimu, au jahanamu? Je, huo hauwezi kuwa upuuzi usio na maana? Nimesema hili mara kadhaa lakini ninyi bado hamwelewi Ninachomaanisha. Ikilinganishwa na jahanamu, Kuzimu imepotoshwa zaidi na Shetani. Wale ambao ni wa Kuzimu ndio walio katika hali mbaya sana, na Sijawaamulia kabla watu hawa kabisa; wale walio wa jahanamu ni wale Niliowaamulia kabla, lakini kisha wameondolewa. Kwa maneno rahisi, Sijamchagua hata mmoja wa watu hawa.

Watu mara nyingi hujionyesha kuwa wataalam katika kutoelewa maneno Yangu. Kama Singeonyesha wazi wazi na kufafanua mambo kidogo kidogo, nani kati yenu angeelewa? Ninyi mnaamini tu nusu hata ya maneno Ninayozungumza, sembuse mambo ambayo hayajatajwa hapo awali. Sasa, migogoro ya ndani imeanza ndani ya mataifa yote: Wafanyakazi wakibishana na

viongozi, wanafunzi na walimu, wananchi na maofisa wa jeshi wa serikali, na shughuli zote kama hizi zinazosababisha vurugu kwanza zinaibuka katika kila taifa, na yote ni sehemu moja tu inayotoa huduma Kwangu. Na kwa nini Nasema inanitolea huduma? Je, Ninafurahia bahati mbaya ya watu? Je, Ninakaa bila kusikiza? Bila shaka hapana! Kwa maana huyu ni Shetani akishambulia katika maumivu makuu ya mwisho ya kifo, na kutoka kwa upande hasi, hii inafanya kazi kama foili^[a] ya mamlaka Yangu na kama foili^[a] ya matendo Yangu ya ajabu. Yote ni ushuhuda wa nguvu ambao unanishuhudia Mimi, na ni silaha ambayo inatumika kumshambulia Shetani. Wakati tu mataifa yote ya dunia yanapigania ardhi na ushawishi, wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi tunatawala kama wafalme pamoja na kuyashughulikia, na inazidi kabisa mawazo yao kwamba chini ya mazingira haya mabaya, ufalme Wangu unafanikishwa kabisa kati ya mwanadamu. Zaidi ya hayo, wanapong’ang’ania mamlaka na wanatamani kuwahukumu wengine, wengine huwahukumu na wao huteketezwa kwa ghadhabu Yangu—ya kusikitisha jinsi gani! Ya kusikitisha jinsi gani! Ufalme Wangu umefanikishwa miongoni mwa wanadamu—ni tukio la kupendeza kweli!

Kuwa mwanadamu (iwe ni watu wa ufalme Wangu au uzao wa Shetani), lazima nyote muone matendo Yangu ya ajabu, vinginevyo Sitalipumzisha jambo hili kamwe. Hata kama uko tayari kukubali hukumu Yangu, bado haitakubalika kama hujaona matendo Yangu ya ajabu. Watu wote lazima washawishike kwa moyo, kwa neno na kwa kuona, na hakuna mtu anayeweza kuruhusiwa kupenyeza tu. Watu wote lazima wanipe Mimi utukufu. Mwishowe, Nitalifanya hata joka kubwa jekundu liinuke na kunisifu kwa ajili ya ushindi Wangu. Hii ni amri Yangu ya utawala—je, utaikumbuka? Watu wote lazima wanisifu bila kukoma na kunipa utukufu!

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Sura ya 91

Roho Wangu huongea na kutamka sauti Yangu daima—wangapi kati yenu wanaweza kunijua Mimi? Kwa nini lazima Nipate mwili na kuja kati yenu? Hili ni fumbo kubwa. Ninyi mnanifikiria kuhusu Mimi na kunitamani sana siku nzima, na mnanisifu, kunifurahia na kunila na kuninywa kila siku, na ilhali leo bado hamnijui Mimi. Ninyi ni wajinga na vipofu kweli! Jinsi gani mnavyonijua kidogo! Ni wangapi kati yenu wanaweza kufikiria kuhusu mapenzi Yangu? Yaani, ni wangapi kati yenu wanaoweza kunijua? Ninyi nyote ni wenye hila, watu wenye nia mbovu, na ilhali bado mnataka kuyaridhisha mapenzi Yangu? Sahau kuhusu hilo! Ninakwambia, bila kujali jinsi vitendo vya Shetani vilivyo vyema, vyote vinafanyika kubomoa ujenzi Wangu na kukatiza usimamizi Wangu. Haijalishi jinsi anavyotenda vizuri, kiini chake hakibadiliki—kinanikana. Kwa hiyo, watu wengi bila kujua hupigwa chini na mkono Wangu na bila kujua

wanaondolewa kutoka kwa familia Yangu. Leo, hakuna jambo hata moja (liwe ni kubwa au dogo) linapangwa na mwanadamu na yote yako mikononi Mwangu. Mtu yeyote akisema kuwa vitu vyote viko chini ya udhibiti wa mwanadamu basi Nakwambia kuwa wewe unanipinga, na Mimi hakika Nitakuadibu vikali na kukuacha bila mahali pa kupumzisha kichwa chako kamwe. Nini, kati ya kila kitu, hakijashikwa ndani ya mikono Yangu? Ni nini kisichopangwa na Mimi, au kuamuliwa na Mimi? Na bado unazungumza kuhusu kunijua Mimi! Huo ni uwongo ulio wazi. Umewadanganya wengine kwa hivyo unadhani unaweza kunidanganya Mimi pia? Unafikiri kwamba iwapo hakuna mtu anayejua kile ambacho umefanya, basi hakuna kitakachofanyika? Usifikiri kuwa utaponea kwa urahisi hivyo! Lazima Nikufanye upige magoti mbele Yangu na kuzungumza wazi. Haikubaliki kutozungumza; hii ni amri Yangu ya utawala!

Je, mnaelewa kwa kweli Roho Wangu ni nani, na mwanadamu Niliye ni nani? Ni nini umuhimu wa Mimi kupata mwili? Ni nani kati yenu ametafakari kwa makini jambo muhimu kama hili na amepokea ufunuo fulani kutoka Kwangu? Ninyi nyote mnajidanganya wenyewe! Kwa nini Nasema kuwa wewe ni mtoto wa joka kubwa jekundu? Leo Nakufichulia fumbo la kupata mwili Kwangu, fumbo ambalo mwanadamu hajakuwa na uwezo wa kufunua tangu kuumbwa kwa ulimwengu, ambalo limewaleta walengwa wengi wa chuki Yangu uharibifu. Na ni hivyo leo. Kwa sababu ya mwili Wangu, wengi ambao Nawapenda wamekamilishwa. Kwa nini hasa lazima Nipate mwili? Na kwa nini Nina umbo Langu la sasa (vitu vyote kama urefu Wangu, sura Yangu na kimo Changu nk)? Nani anayeweza kusema jambo moja kuhusu hilo? Kuna umuhimu mkubwa sana kwa kupata mwili Kwangu kiasi kwamba hauwezi kusemwa wote kabisa. Nitawaambia sasa sehemu yake tu (kwa kuwa hatua za kazi Yangu zimefika umbali huu, hivyo ni lazima Nifanye hivi na kusema hivi): Kupata mwili Kwangu kunaelekezwa kimsingi kwa wazaliwa Wangu wa kwanza, ili Nipate kuwachunga na ili waweze kuzungumza na kuongea uso kwa uso na Mimi; inaonyesha zaidi kwamba Mimi na wazaliwa Wangu wa kwanza ni wandani sisi kwa sisi (kumaanisha kwamba tunakula pamoja, kukaa pamoja, kuishi pamoja na kuchukua hatua pamoja), ili kwamba waweze kulishwa na Mimi kwa kweli—haya si maneno matupu ila ni ukweli. Hapo awali, watu waliniamini lakini hawakuweza kufahamu ukweli, na hii ilikuwa kwa sababu Sikuwa nimepata mwili bado. Leo, kupata mwili Kwangu kunawawezesha nyote kuelewa hali halisi na kunawaruhusu wale ambao wananipenda kwa dhati kunijua kupitia kwa usemi Wangu na mwenendo Wangu na kanuni za jinsi Ninavyoshughulikia mambo—Mungu mwenye hekima Mwenyewe. Pia kunaruhusu wale ambao hawanitafuti kwa dhati kuona kipengele cha Mimi ambacho ni ubinadamu Wangu katika vitendo Vyangu visivyofikiriwa na hivyo kunipinga, na kisha kufa “bila sababu yoyote,” wakipigwa chini na Mimi. Katika kumdhalilisha Shetani, kupata mwili kunakuwa na ushahidi wa nguvu zaidi Kwangu; sio tu kwamba Naweza kutoka katika mwili lakini pia Naweza kuishi ndani ya mwili. Sipitii kizuizi

cha hewa au kijiografia, na Mimi hakuna vizuizi vyovyote kabisa na kila kitu kinapita vizuri. Shetani anaaibishwa zaidi na hoja hii, na Ninapotoka katika mwili, bado Nafanya kazi kupitia kwa mwili Wangu, na Siathiriwi hata kidogo. Bado Natembea juu ya milima, mito, maziwa, na kila pembe ya ulimwengu, na vile vile vitu vingi ndani yake. Nimepata mwili ili kuwafichua wale wote waliozaliwa kutoka Kwangu lakini ambao wameinuka kunipinga. Nisingekuwa mwili, hakungekuwa na njia ya kuwafichua (kumaanisha wale wanaotenda kwa njia moja mbele Yangu na kwa njia nyingine nyuma Yangu). Kama Ningebaki kama Roho, watu wangeniabudu katika dhana zao, na wangefikiria kuwa Mimi ni Mungu asiye na umbo na asiyeweza kufikiwa. Nimepata mwili leo kama kinyume cha dhana za watu (kuzungumzia urefu na sura Yangu), kuonekana kama mtu wa kawaida na kutokuwa mrefu sana. Ni jambo hili ambalo humdhalilisha Shetani zaidi na ni kinyume cha nguvu zaidi kwa dhana za watu (kufuru ya Shetani). Kama sura Yangu ingekuwa tofauti na kila mtu basi hilo lingekuwa tatizo—kila mtu angekuja kuniabudu na kunielewa kupitia kwa dhana zao wenyewe, na hawangeweza kuwa na ushahidi huo mzuri Kwangu. Kwa hiyo Nilijichukulia Mwenyewe umbo Nililo nalo leo, na si vigumu kuelewa hata kidogo. Kila mtu anapaswa kutoka nje ya dhana za binadamu na kutopotoshwa na njama za hila za Shetani. Katika siku zijazo Nitawaambia zaidi kwa mfululizo, kulingana na mahitaji ya kazi Yangu.

Leo, mradi Wangu umefanikiwa na mpango Wangu umekamilika. Nimelipata kundi la watu wanaoshirikiana na Mimi kwa akili na mawazo sawa. Huu ndio wakati mtukufu zaidi Kwangu. Wanangu wapendwa (wale wote wanaonipenda) wanaweza kuwa wenye moyo na akili moja na Mimi katika kukamilisha mambo yote ambayo Nahitaji kufanya pamoja na Mimi—hili ni jambo la ajabu. Baada ya leo, wale Nisioridhika nao hawatakuwa na kazi ya Roho Mtakatifu. Yaani, Nitawaondoa wale ambao hawapatani na kile ambacho Nimesema hapo awali. Watu lazima wapataane kikamilifu na kile Ninachosema. Kumbuka hili! Ni kupatana kikamilifu. Usielewe visivyo; yote ni juu Yangu. Watu, msizungumze masharti na Mimi. Nikisema unastahili basi haitabadilika, na Nikisema kuwa wewe hustahili, usionekane mwenye uchungu na kulaumu Mbingu na dunia—yote ni mipangilio Yangu. Ni nani aliyekufanya ujikosee heshima? Nani aliyekufanya utende lile kosa la aibu? Hata kama husemi lolote huwezi kuficha ukweli kutoka Kwangu. Nani Ninayemlenga ninaposema Mimi ni Mungu Mwenyewe ambaye anachunguza moyo wa ndani kabisa wa mwanadamu? Nawaambia wale wasio waaminifu. Kufanya jambo kama hilo nyuma Yangu, hamna aibu sana. Je, mnataka kunidanganya? Si rahisi vile! Ondokeni hapa mara moja! Mwana wa uasi! Hujipendi mwenyewe, na hujiheshimu mwenyewe! Wewe hujali kujihusu mwenyewe, lakini bado unataka Mimi nikupende? Sahau hilo! Sitaki hata mmoja wa fidhuli kama hao. Wote watatoka hapa! Hili huleta aibu kubwa zaidi juu ya jina Langu na halitakubalika kwa ninyi kutoona jambo hili wazi. Lazima mjilinde kutokana na kutiwa najisi na

uchafu wowote katika enzi hii nzee ya uovu na uzinzi; lazima muwe watakatifu kabisa na msio na dosari. Leo, wale walio na sifa za kutosha kutawala kama wafalme pamoja na Mimi ni wale ambao hawajatiwa najisi na uchafu wowote, kwa maana Mimi ni Mungu mtakatifu Mwenyewe na Simtaki yeyote anayeliaibisha jina Langu. Watu kama hawa wametumwa na Shetani kunijaribu, na hakika wao wote ni watumishi wa Shetani ambao wanapaswa kupigwa pia (kuwatupa kwenye shimo lisilo na mwisho).

Familia Yangu ni takatifu na isiyo na dosari, na hekalu Langu ni kubwa na adhimu (kumaanisha wale walio na kile Nilicho na kile Nilicho nacho). Ni nani anayethubutu kuingia na kusababisha vurugu bila mpango? Bila shaka Sitamsamehe. Ataangamizwa kabisa na lazima aabishwe kabisa. Natenda kwa busara. Bila kisu, bila bunduki na bila juhudi yoyote, Nitawashinda kabisa wale wanaonipinga na kuliaibisha jina Langu. Mimi ni karimu, na kwa kasi thabiti Naendelea na kazi Yangu hata wakati Shetani anasababisha usumbufu kama huo; Simjali na Nitamshinda kwa ukamilishaji wa mpango Wangu wa usimamizi. Hii ni nguvu Yangu na hekima Yangu, na hata zaidi ni sehemu ndogo ya utukufu Wangu usioisha. Machoni Pangu, wale wanaonipinga Mimi ni kama wadudu wanaotambaa mchangani na, kama Ninavyotamani ambao naweza kuwavunja hadi kufa chini ya mguu kulingana na nia Zangu, wakati wowote. Hata hivyo, Mimi hufanya mambo kwa hekima. Nataka wazaliwa Wangu wa kwanza waende wawashughulikie; Mimi siko katika haraka. Natenda kwa mpangilio, kwa hali ya utaratibu, na kwa usahihi bila makosa yoyote. Hao wazaliwa wa kwanza ambao wamezaliwa kutoka Kwangu wanapaswa kumiliki kile Nilicho, na waweze kuona hekima Yangu isiyoisha katika matendo Yangu!

Sura ya 92

Kila mmoja anaweza kuuona uweza Wangu na hekima Yangu ndani ya maneno Ninayoyazungumza na mambo Ninayoyatenda. Popote Ninapokwenda, kazi Yangu iko pale. Hatua Zangu haziko nchini China pekee, bali muhimu zaidi, ziko katika mataifa yote ya dunia. Ya kwanza kulipokea jina hili, hata hivyo, ni mataifa saba tu ambayo yamezungumziwa hapo awali, kwani hizi ni hatua za kazi Yangu, na hivi karibuni mtaweza kufahamu kabisa kuihusu na mtaielewa kabisa. Nikiwaambia sasa, Nina wasiwasi kuwa wengi wataanguka chini, kama Nilivyosema awali kuwa Ninazungumza nanyi na kutamka sauti Yangu kulingana na vimo vyenu, na kila kitu Ninachofanya kina hekima Yangu isiyo na mwisho ndani yake ambayo hakuna mtu anayeweza kuifahamu; Ninaweza tu kuwaambia kuihusu kidogo kidogo kwa wakati. Jueni hili! Nyinyi daima ni watoto machoni Pangu; kwa kila hatua mnayochukua mnapaswa kuongozwa na Mimi na kuelekezwa na Mimi. Watu, ni chini ya uongozi Wangu tu ndipo mnaweza kupitia maisha yenu yote, vinginevyo hakuna mtu ambaye angeweza kuendelea kuishi.

Ulimwengu dunia wote uko mikononi Mwangu, lakini hunioni Nikihangaika hapa na pale. Kinyume chake, Mimi ni mwenye utulivu na furaha. Watu hawajui uweza Wangu na wote wanatamani kuhisi wasiwasi kwa niaba Yangu—mnajua kidogo sana kujihusu! Bado mnaonyesha takataka zenu mbele Zangu, mkijisifu wenyewe! Nilielewa hili kitambo. Na mnajishughulisha na udanganyifu mbele Zangu, nyinyi mafidhuli wa kudharaulika! Toka nyumbani Mwangu sasa hivi! Sitaki vitu kama nyinyi. Ni heri Nisiwe na mtu yeyote katika ufalme Wangu hata kidogo, kuliko kutaka mafidhuli wa kudharaulika wa aina yenu! Je, wewe unajua kwamba tayari Sifanyi kazi juu yako? Licha ya ukweli kwamba bado unakula na kuvaa kama kawaida! Lakini je, unajua kwamba wewe huishi kwa ajili ya Shetani? Kuwa unatoa huduma kwa Shetani? Na bado una ujasiri wa kusimama mbele Yangu! Wewe huna aibu kabisa!

Hapo awali, mara nyingi Nilisema, “Maafa makubwa yatakuja hivi karibuni; maafa makubwa tayari yameanguka kutoka kwa mikono Yangu.” Je, “maafa makubwa” yanamaanisha nini, na hili “yameanguka” linapaswa kuelezwa vipi? Mnafikiri kuwa maafa haya makubwa yanamaanisha maafa yasiyoepukika ambayo hudhuru roho ya wanadamu, nafsi na mwili, na mnafikiri kuwa “mitetemeko ya ardhi, njaa na mateso” ambayo Ninayazungumzia ndiyo maafa haya makubwa. Lakini msichojua ni kwamba mmeelewa vibaya maneno Yangu. Na mnafikiri kuwa hili “yameanguka” lina maana kwamba maafa makubwa yameanza; hili linachekesha! Yaani mnaielewa kwa njia hii, na baada ya kusikia maelezo yenu Ninakasirika sana. Fumbo ambalo watu hawajaweza kufumbua (fumbo la siri zaidi) pia ndilo fumbo ambalo limeeleweka vibaya sana katika enzi zote. Zaidi ya hayo, fumbo hili ni jambo ambalo hakuna aliyewahi kulipitia hapo awali (kwani fumbo hili litatimizika tu katika siku za mwisho, na katika enzi ya mwisho tu ndipo wanadamu wanaweza kuliona lakini hawalijui) kwa sababu Nimelifunga kabisa na wanadamu hawawezi kulipenyeza kabisa (hawawezi kuona hata sehemu yake ndogo zaidi). Kwa kuwa kazi Yangu imeendelea hadi hatua hii, ninawatia msukumo kulingana na mahitaji ya kazi Yangu, vinginevyo hamngekuwa na njia ya kuelewa. Sasa Ninaanza ushirika na kila mtu anapaswa kuzingatia, vinginevyo yeyote asiye mwangalifu, ikiwa ni pamoja na wazaliwa Wangu wa kwanza, atakabiliwa na hukumu Yangu, na katika hali mbaya zaidi atapigwa kwa mkono Wangu (kumaanisha kwamba roho, nafsi na mwili wake vitachukuliwa). Maafa makubwa yanazungumziwa kuhusiana na kila amri ya utawala wa ufalme Wangu, na kila moja ya amri Zangu za utawala ni sehemu ya maafa makubwa. (Amri Zangu za utawala hazijafunuliwa kabisa kwenu, lakini msiwe na hofu au wasiwasi juu ya hili; kuna baadhi ya mambo ambayo yatawaletwa manufaa madogo mkiyajua mapema zaidi. Kumbukeni hili! Mimi ni Mungu mwenye hekima.) Je, sehemu nyingine ni gani? Maafa makubwa yana sehemu mbili: Amri Zangu za utawala na hasira Yangu. Wakati ambapo maafa makubwa yataanguka utakuwa pia wakati ambapo Nitaanza kutenda kwa hasira na kutekeleza amri Yangu ya utawala. Hapa

Ninawaambia wana Wangu wazaliwa wa kwanza: Lazima mhakikishe kuwa hamtadhoofika kutokana na hili. Je, mmesahau kwamba vitu vyote na mambo yote yameamuliwa awali na Mimi? Mwana Wangu, usiogope! Hakika Mimi nitawahifadhi, mtafurahia baraka nzuri na Mimi milele, na mtakuwa pamoja nami milele. Kwa sababu nyinyi ni wapendwa Wangu, Sitawaacha; kwa sababu Sifanyi mambo ya upumbavu, Nikibomoa kitu ambacho kimekamiliwa kwa ugumu, je, si itakua kujichoma mguuni? Ninajua unachofikiria katika moyo wako. Umekumbuka? Nini kingine ungependa Mimi niseme? Nitazungumza zaidi juu ya maafa makubwa. Wakati ambapo maafa makubwa yatafika utakuwa wakati wa kutisha zaidi na yatafichua zaidi uovu wa mwanadamu. Kila aina ya sura ya mapepo itafichuliwa kwa mwanga wa uso Wangu na hawatakuwa na mahali pa kujificha, mahali popote pa kupata kivuli; watafichuliwa kabisa. Matokeo ya maafa makubwa yatakuwa kuwafanya wale wote ambao sio wateule Wangu au sio Niliowaamulia awali kupiga magoti mbele Zangu na kuomba msamaha, kwa kutoa machozi na kusaga meno. Hii ni hukumu Yangu ya Shetani, hukumu Yangu ya ghadhabu. Kwa sasa Ninafanya kazi hii na labda kuna watu ambao wanapenda kujifanya kuwa na uwezo na kutumia njia ya udanganyifu, lakini kadri wanavyozidi kuwa hivi ndivyo Shetani atazidi kufanya kazi juu yao, mpaka wafikie hatua ambapo hali zao za awali zinafichuliwa.

Sina haraka katika kufanya kazi Yangu, na Ninampanga kila mtu Mimi Mwenyewe (hii inawadhihaki na inathibitisha kuwa wao ni wazao wa joka kubwa jekundu na Siwasikilizi, kwa hiyo kutumia “kupanga” sio kuzidi), na kufanya kila kazi Mimi Mwenyewe. Kila kitu kinafanikiwa na Mimi, na ni mafanikio salama salimini; kila kitu Ninachofanya, hatua kwa hatua, tayari imepangwa. Nawaambieni mapenzi Yangu na kuhusu mzigo Wangu kidogo kidogo kwa wakati. Kuanzia wakati huu, maneno Yangu yanaanza kuonekana kwa mataifa yote na watu wote. Kwa sababu wana Wangu wazaliwa wa kwanza tayari wamefanywa kuwa kamili(lengo la maneno Yangu ni wana Wangu na watu Wangu), njia ambayo Mimi hufanya kazi imeanza kubadilika tena. Je, mnaelewa hili vizuri? Je, mmesikia toni ya maneno Yangu hizi siku chache zilizopita? Ninawafariji wana Wangu wazaliwa wa kwanza kila hatua ya njia, lakini kuanzia sasa (kwa sababu wana Wangu wazaliwa wa kwanza tayari wamefanywa kuwa kamili) Mimi hubeba kisu mkononi Mwangu (kuwa maneno ya ukali zaidi). Mtu yeyote ambaye Mimi humtazama kwa wakati kama asiyefaa (kumaanisha wale ambao hawajaamuliwa awali au kuchaguliwa, kwa hivyo hakuna ukinzani), Sijali kama wanatoa huduma Kwangu, au kama wao ni kitu kingine, Nitawaondoa mara moja. Mimi ni Mwenyezi Mungu na Ninaweza kuwafanya watu wote wanihudumie. Sisiti kutengana na mtu wa aina hiyo hata kidogo; Nikisema simtaki basi simtaki. Sasa kwa kuwa wakati huu umefika, Ninahitaji tu kumwona mtu anayenichukiza na Nitamtupa mara moja bila uchunguzi. Kwa sababu Mimi ni Mungu ambaye anafuata neno Lake. Kwa wale ambao Nimewaamulia awali kuwa katika utumishi Wangu, bila kujali wema wako au kama

umefanya chochote kinachonikaidi au la, ukinichukiza basi Nitakutimua. Mimi siogopi matatizo ya baadaye. Nina amri Zangu za utawala, ninafuata neno Langu na neno Langu litatimia. Je, Ninaweza kumweka Shetani? Nisikilizeni, enyi watu! Si lazima uogope; ni lazima uondoke wakati wowote Ninapokwambia uondoke. Usinipe visingizio kwani Mimi sina maneno ya kukuambia! Kwa sababu Nimekuwa na uvumilivu kama huo, na wakati wa kutekeleza amri Zangu za utawala umefika na siku yenu ya mwisho pia imewadia. Kwa maelfu ya miaka mlipotoshwa na daima mkafanya mambo kwa njia ya ukaidi na ya makusudi, lakini siku zote Nilikuwa na subira (kwa sababu Mimi ni mkarimu na huuruhusu upotovu wako ufikie kiasi fulani). Lakini sasa tarehe ya mwisho ya huruma Yangu imefika na wakati umefika kwenu kumilikiwa na kutupwa katika ziwa la moto na kiberiti. Fanyeni hima na muondoke njiani. Ninaanza kutekeleza rasmi hukumu Yangu na kuachilia hasira Yangu.

Katika mataifa yote na maeneo yote ya dunia, mitetemeko ya ardhi, njaa, maafa, kila aina ya maafa hutokea mara kwa mara. Ninapofanya kazi Yangu kubwa katika mataifa yote na maeneo yote, maafa haya yatatokea kwa ukali zaidi kuliko wakati mwingine wowote tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Huu ndio mwanzo wa hukumu Yangu ya watu wote; lakini wana Wangu wanaweza kupumzika bila wasiwasi, hakuna janga litakalowakumba, nami Nitawahifadhi (kumaanisha kuwa nyinyi baadaye mtakuwa hai katika mwili, lakini si katika nyama na damu, hivyo hamtaweza kuteseka na maumivu ya janga lolote). Nyinyi mtakuwa tu pamoja na Mimi mkitawala kama wafalme na kuyahukumu mataifa yote na watu wote, kufurahia baraka nzuri na Mimi milele katika dunia na miisho ya ulimwengu. Maneno haya yote yatatimizwa na hivi karibuni yatafanikishwa mbele ya macho yenu. Sichelewi hata saa moja au siku moja, Mimi hufanya mambo haraka sana. Usiwe na hofu au wasiwasi, na baraka Ninayokupa ni kitu ambacho hakuna mtu anayeweza kukunyang'anya—hii ni amri Yangu ya utawala. Watu wote watanitii kwa sababu ya matendo Yangu; sio kwamba watashangilia na kushangilia tu, lakini hata zaidi watarukaruka kwa furaha.

Sura ya 93

Ukweli unatimizwa mbele ya macho ya mtu na mambo yote yametimizwa. Kazi Yangu inapata hatua, ikipanda juu kama roketi iliyofyatuliwa, ambayo hakuna mtu aliwahi kutarajia. Ni baada ya vitu kufanyika ndipo mtaelewa maana ya kweli ya maneno Yangu. Watoto wa joka kubwa jekundu si wa pekee na lazima wafanywe kushuhudia matendo Yangu ya ajabu kwa macho yao wenyewe. Usidhani kwamba Sitakutelekeza, sasa kwa kuwa una uhakika kunihusu baada ya kuona matendo Yangu—si rahisi hivyo! Yote ambayo Nimesema na mambo ambayo Nimeamua hakika Nitatimiza, na hayatarudi Kwangu yakiwa matupu. Nchini China, kando na walio wachache ambao ni wazaliwa Wangu wa kwanza, kuna wachache ambao ni watu Wangu.

Kwa hivyo leo Nasema wazi kwenu (watoto wa joka kubwa jekundu, ambao wamenitesa vibaya sana) kwamba lazima msishikilie matumaini yoyote makubwa, na kwamba lengo la kazi Yangu (tangu uumbaji wa dunia) limekuwa kwa wazaliwa Wangu wa kwanza na kwa mataifa kadhaa nje ya Uchina. Kwa sababu hii, wakati wazaliwa Wangu wa kwanza wamekomaa, mapenzi Yangu yatatimizwa. (Punde wazaliwa Wangu wa kwanza wamekomaa, mambo yote yatafanyika, kwa kuwa kazi iliyo mbele imepewa wao.) Sasa Naruhusu watu hawa kuona sehemu ya matendo Yangu ya ajabu ili tu kwamba joka kubwa jekundu liaibishwe. Watu hawa hawawezi kabisa kupata raha katika hilo ila wanaweza tu kufurahi kwamba wananitolea huduma. Na hawana mbadala, kwa kuwa Nina amri Zangu za utawala na hakuna anayethubutu kuzikosea.

Sasa Nitashiriki kuhusu hali zinazohusiana na kuja kwa wageni, ili mweze kuzijua kabla zitokee, mtayarishe kila kitu vizuri ili kushuhudia jina Langu, na kuwa juu yao na kuwatawala. (Kwa sababu mkubwa zaidi kati yao bado ndiye mdogo zaidi miongoni mwenu, Nasema ninyi muwe juu yao na kuwatawala.) Watu hawa wote wamepata ufunuo wa Roho Mtakatifu na baadaye wote watakusanyika Uchina, kana kwamba kwa mpango wa kabla. Joka kubwa jekundu linastuliwa na linajaribu kufanya kila linaloweza kupinga, lakini kumbukeni jambo moja! Mpango Wangu wa usimamizi umetimika kabisa, na hakuna kitu na hakuna mtu anayethubutu kuzuia hatua Zangu. Ninawapa ufunuo kila wakati, na wanatenda kwa kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu. Bila shaka hawatateseka vifungo vya joka kubwa jekundu, kwa kuwa nami yote ni ufunguliwaji na uhuru. Nimepanga mambo yote kwa njia ya kufaa, Nikiwangoja mwandae kazi ya matayarisho kuwaongoza. Nimesema hili daima kwenu zamani, lakini wengi wenu mnaamini kwa njia nusu bado. Hali ni gani sasa? Mmepigwa na bumbuazi, sivyo?

Mambo haya yote ni ya baadaye; jambo kuu ni kwenu kuandaa kazi yote ya matayarisho haraka iwezekanavyo. Msishtuke. Yule anayefanya kazi ni Mimi na, wakati utakapofika, Nitafanya kazi Yangu Mwenyewe. Nimelivunja joka kubwa jekundu vipande vipande. Yaani, Roho Wangu ametoka kwa watu wote isipokuwa wazaliwa Wangu wa kwanza (sasa kuifanya kuwa rahisi zaidi kufichua nani ni watoto wa joka kubwa jekundu). Watu hawa wamemaliza kunitolea huduma na Nitawatuma tena kwa shimo lisilo na mwisho. (Inamaanisha kwamba Sitamtumia hata mmoja wao. Kutoka sasa kuendelea wazaliwa Wangu wa kwanza watafichuliwa kabisa na wale ambao wako kando Yangu na wanaofaa kwa matumizi Yangu watakuwa wazaliwa Wangu wa kwanza.) Wazaliwa Wangu wa kwanza, mnafurahia kirasmi baraka Ninazowapa (kwa kuwa wale Ninaowachukia sana wameonyesha tabia yao ya kweli), na kuanzia hapo na kuendelea hakuna kitu kitakachofanyika tena na ninyi ambacho kinaniasi. Mna uhakika asilimia mia moja kunihusu. (Ni leo tu ndipo hili linakamilishwa kikamilifu, na Nilikuwa nimeagiza kabla wakati huu.) Yote mnayofikiri mioyoni na akilini mwenu ni upendo usio na mwisho Kwangu, uchaji Kwangu, na mnanisifu na kunitukuza nyakati zote. Kweli mnaishi chini

ya utunzaji na ulinzi wa upendo Wangu, mkiishi katika mbingu ya tatu. Furaha na ridhaa kubwa isiyo na kifani! Ni ufalme mwingine ambao watu wanaona kuwa mgumu kufikiria—dunia ya roho ya kweli!

Maafa yote yanaibuka kwa kufuatana, kila likiwa kali kuliko la awali, na hali inakuwa yenye wasiwasi kila siku. Huu ni mwanzo tu wa maafa, na maafa makali zaidi ambayo yatakuja baadaye hayafikiriki kwa mwanadamu. Acha wanangu wayashughulikie: hii ni amri Yangu ya utawala na ndiyo Niliyopanga kitambo. Ishara na maajabu yote, ambayo hayajawahi kuonwa awali na mwanadamu, huibuka kutoka Kwangu, yakionekana moja baada ya lingine kwa kila mtu (kumaanisha watu wote wa ufalme Wangu). Lakini hili ni jambo ambalo litafanyika katika siku za baadaye za karibu. Msiwe na wasiwasi. Watu wote wamezungumza awali kuhusu kuingia katika ufalme, kwa hivyo hali za kuingia katika ufalme ni zipi? Na ufalme ni nini? Ni mji yakinifu? Mnaelewa visivyo. Ufalme hauko duniani, wala hauko katika mbingu yakinifu, lakini badala yake ni dunia ya roho ambayo haiwezi kuonwa au kuguswa na mwanadamu. Ni wale tu ambao wanafanywa kuwa kamili kabisa na Mimi na kufurahia baraka Zangu baada ya kukubali jina Langu wataweza kuingia ndani. Dunia ya roho ambayo imetajwa awali mara nyingi ni sehemu ya juu ya ufalme. Kuingia katika ufalme kwa kweli, hata hivyo, si jambo rahisi. Wale ambao wanauingia lazima wapate ahadi Yangu na lazima wawe watu ambao Nimewajaalia na kuwachajua Mwenyewe. Kwa hivyo dunia ya roho si mahali ambapo watu wanaweza kuja na kuenda watakavyo. Ufahamu wa watu wa hili ulikuwa wa juu juu sana na ilikuwa dhana ya mwanadamu tu. Wale wanaoingia katika ufalme tu ndio wanaoweza kufurahia baraka, kwa hivyo baraka hizi haziwezi kufurahiwa na mwanadamu tu, lakini hata zaidi haziwezi kuonekana, na hii ndiyo amri Yangu ya mwisho ya utawala.

Sura ya 94

Narudi Sayuni pamoja na wazaliwa Wangu wa kwanza—kweli mnaelewa maana ya kweli ya maneno haya? Nimewakumbusha tena na tena kwamba Mimi nataka mkue haraka ili mtawale na Mimi. Je, mnakumbuka? Vitu hivi vyote vinahusiana moja kwa moja na kupata mwili Kwangu. Kutoka Sayuni Nilikuja duniani katika nyama ili Nipate kupitia nyama kundi la watu ambao ni wa akili moja na Mimi, na kisha turudi Sayuni. Hili linamaanisha kwamba tutarudi kutoka kwa nyama hadi kwa mwili wa awali. Hii ndiyo maana ya kweli ya “kurudi Sayuni.” Hii pia ndiyo maana ya kweli na lengo la mpango Wangu mzima wa usimamizi, na hata zaidi sehemu muhimu zaidi ya mpango Wangu wa usimamizi, ambayo hakuna anayeweza kuizuia, na ambayo itatimizwa mara moja. Kama nyinyi mko katika nyama hamtawahi kamwe kuondoa mawazo na fikira za binadamu, sembuse kutupa mbali hewa ya kidunia, kutoa vumbi, na nyinyi daima mtakuwa udongo; ni wakati mko katika mwili tu ndio mtastahiki kufurahia baraka. Je,

baraka ni nini? Je, mnakumbuka? Katika mwili hakuwezi kuwa na fikira ya baraka, hivyo kila mwana wa kwanza kuzaliwa lazima afuate njia kutoka kwa nyama hadi kwa mwili. Katika nyama mnadhulumwa na kuteswa na joka kubwa jekundu (hii ni kwa sababu nyinyi hamna nguvu, hamjapata utukufu wowote), lakini katika mwili itakuwa tofauti sana, na mtajivunia na kuwa na furaha: Siku za kukandamizwa zitaenda kabisa na nyinyi daima mtakuwa mmefunguliwa na kuachwa huru. Lazima iwe hivi kama Ninafaa kuongeza kile Mimi Nilicho na kile Ninacho ndani yenu. Vinginevyo, nyinyi mtakuwa tu na sifa Zangu. Haijalishi jinsi mtu huiga mtu mwingine kwa nje, hawawezi kuwa sawa kabisa. Katika mwili mtakatifu wa kiroho tu (hii inarejelea mwili) ndio tunaweza kuwa sawa kabisa. (Hii inarejelea kuwa na sifa sawa, kuwa na nafsi sawa, mali sawa, na kuweza kuwa wenye mawazo sawa, kuungana, bila kugawanyika na kutengeka, kwa kuwa yote ni mwili mtakatifu wa kiroho).

Kwa nini sasa mnaanza kuchukia dunia, na kuchukizwa na kila aina ya mambo yanayokera kama kula, kuvaa, na kadhalika, na msiweze kusubiri kuzitupa mbali? Hii ndiyo ishara kwamba mtaingia katika dunia ya kiroho (mwili), na nyinyi nyote mna jakamoyo ya haya (ingawa si wote kwa kiwango sawa). Nitatumia kila aina ya watu tofauti, matukio tofauti, na mambo tofauti kutumikia hatua Yangu muhimu zaidi, na yote yatatoa huduma kwa ajili Yangu. Lazima Nifanye hivyo. (Bila shaka Mimi siwezi kukamilisha hili katika nyama, na Roho Wangu mwenyewe tu ndiye Anayeweza kufanya kazi hii, kwa sababu wakati haujasili.) Hii ndiyo sehemu ndogo ya mwisho ya kazi kwa ajili ya ulimwengu dunia wote. Kila mtu atanisifu na kunipokea Mimi kwa shangwe. Kazi Yangu kuu ni kamili: Vitasa saba vya mapigo vinamwagika kutoka mkono Wangu, ngurumo saba zinatoa sauti, mabaragumu saba yatoa sauti, na mihuri saba inafunguliwa, kwa ulimwengu dunia, kwa mataifa yote na watu wote, na kwa milima, mito na kila kitu. Je, vitasa saba vya mapigo ni vipi? Je, vimeelekezwa kwa nini? Kwa nini Ninasema kwamba vitamwagika kutoka kwa mkono Wangu? Muda mrefu utapita kabla ya kila mtu kuridhishwa, na kabla ya kila mtu kuelewa kabisa. Hata Nikiwaambia sasa nyinyi mtaelewa sehemu ndogo tu. Kulingana na fikira za binadamu, vitasa saba vya mapigo vinaelekezwa kwa nchi zote na watu wote wa dunia, lakini kwa kweli hali haiko hivi. Vitasa hivi saba vya mapigo vinarejelea ushawishi wa Shetani ibilisi na njama ya joka kubwa jekundu (chombo ambacho Mimi hutumia kutoa huduma kwa ajili Yangu). Wakati huo Nitamfungulia Shetani na joka kubwa jekundu kuadibu wana na watu, na hapo litafichuliwa wana ni akika nani na nani ndio watu. Wale ambao wamedanganywa ni wale ambao hawakuwa walengwa wa kujalia Kwangu kabla, huku wazaliwa Wangu wa kwanza kwa wakati huu watakuwa wakitawala na Mimi. Kupitia hili wana na watu wanafanywa wakamilifu. Kumwagika kwa vitasa saba vya mapigo hakutaathiri mataifa yote na watu wote, lakini tu wana Wangu na watu Wangu, Baraka hazikuji rahisi, na gharama nzima lazima ilipwe. Wakati wana na watu watakua vitasa saba vya mapigo vitaondolewa kabisa na

baadaye havitakuwepo. Je, ni nini ngurumo saba zinazotoa sauti? Hili si ngumu kuelewa. Wakati wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi tunakuwa mwili, ngurumo saba zitatoa sauti. Hili litatisika ulimwengu wote, kana kwamba mbingu na dunia zimepinduliwa juu chini. Kila mtu atajua hili, na hakuna mmoja ambaye hatalijua hili. Wakati huo wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi tutakuwa pamoja katika utukufu na tutaanza hatua ifuatayo ya kazi. Watu wengi watapiga magoti kwa ajili ya huruma na msamaha kwa sababu ngurumo saba zinatoa sauti. Lakini hii haitakuwa tena Enzi ya Neema: itakuwa wakati wa ghadhabu. Na kuhusu watu wote watendao uovu (wale ambao huzini, au hujihusisha na fedha chafu, au wana mipaka isiyo wazi kati ya wanaume na wanawake, au ambao hukatiza au kuharibu usimamizi Wangu, au ambao roho zao zimezibwa, au waliopagawa na mapepo mabaya, na kadhalika—wote isipokuwa wateule Wangu), hakuna kati yao ataachiliwa, wala yeyote kusamehewa, lakini wote watatupwa chini Kuzimu na kufa milele! Mabaragumu saba kutoa sauti hakurejelei mazingira makubwa mabaya, wala hakurejelei chochote kutangazwa kwa dunia, ambayo ni dhana ya binadamu kabisa. Mabaragumu saba yanarejelea matamko Yangu ya ghadhabu. Wakati sauti Yangu (hukumu ya adhimu na hukumu ya ghadhabu) inatoka, mabaragumu saba hutoa sauti. (Sasa hivi, nyumbani Mwangu, hili ndilo la nguvu zaidi, ambalo hakuna anayeweza kulitoroka.) Na mapepo wote katika kuzimuni na jahanamu, wakubwa kwa wadogo, watafunika vichwa vyao mikononi mwao na kukimbia kwa pande zote, wakilia na kusaga meno yao, wakiwa na aibu na bilapopote pa kujificha. Kwa sasa si mabaragumu saba yanayoanza kutoa sauti, lakini ni ghadhabu Yangu na pia hukumu Yangu kali zaidi, ambayo hakuna anayeweza kutoroka, na wote lazima wapitie. Kwa wakati huu kile ambacho kimefichuliwa si yaliyomo kwa mihuri saba. Mihuri saba ni baraka mtakayofurahia baadaye. Kile kinachodaiwa kuwa nafasi wazi hurejelea kuwajuza tu, lakini bado hamjafurahia baraka hizi. Wakati mtazifurahia baraka hizi, basi mtajua yaliyomo kwa mihuri saba. Sasa mnagusia tu sehemu ambayo bado si kamili. Naweza tu kuwaambia hatua kwa hatua katika kazi ya baadaye, hivyo mtaipitia binafsi na kuhisi utukufu usioweza kufananishwa, na mtakuwa katika hali ya raha isiyoisha.

Kuwa na uwezo wa kufurahia baraka za wazaliwa wa kwanza si kitu rahisi, wala si kitu mtu wa kawaida anaweza kufikia. Nitahimiza mara moja tena na kusema kwa nguvu zaidi kwamba lazima Niweke mahitaji makali kwa wazaliwa Wangu wa kwanza. Vinginevyo hawawezi kutukuza jina Langu. Nimekataa kwa uthabiti yeyote anaye sifa mbaya duniani, na hata zaidi Ninakataa yeyote ambaye ni mzinzi. (Hawana mgao katika kuwa watu wa Mungu—kuhusu hili Nasisitiza hasa.) Msifikiri kwamba yaliyopita yameenda—kunawezaje kuwa na kitu kizuri hivi! Je, ni rahisi sana kupata hadhi ya wazaliwa wa kwanza? Na kwa njia sawa Nakataa yeyote ambaye ananipinga, yeyote ambaye hanitambui katika mwili Wangu, yeyote ambaye anaingilia kati Ninapofanya mapenzi Yangu, na yeyote ambaye ananitesa—Mimi ni mkali sana (kwa

sababu Nimechukua tena nguvu Yangu kabisa)! Hatimaye, kwa njia sawa Nakataa yeyote ambaye katika maisha yake hajakuwa na vikwazo. Nataka wale ambao, kama Mimi, hutoka katika mateso yao, hata kama ni mateso madogo. Vinginevyo, Nitawafukuza watu kama hawa nje. Msiwe bila aibu, ukitaka kuwa mzaliwa Wangu wa kwanza, ukijionyesha mbele Yangu. Kujeni ghafula kwa haraka kwa upande Wangu! Umeniambia awali mambo ya upuuzi, ukitafula kushinda furaha Yangu! Huu ni upofu! Je, hujui kwamba Nakuchukia wewe, bazazi! Je, unafikiri Mimi sijui biashara yako isiyo halisi? Unajificha tena na tena! Je, hujui kwamba umefichua uso wako wa kishetani? Ingawa watu hawawezi kuuona, unafikiri kwamba Mimi siwezi kuuona? Wale wanaotoa huduma Kwangu si vitu vizuri bali ni kikundi cha mabazazi. Mimi lazima Niwashughulikie na Nitawarusha katika shimo lisilo na mwisho na kuwachoma!

Mtu ambaye huongea kwa njia isiyo ya kumcha Mungu, anayetenda bila imani, na ambaye hashirikiani na wengine vizuri, mtu kama huyu angetaka kuwa mfalme. Je, wewe huoti ndoto? Je, wewe hujadanganyika? Je, wewe huoni ulicho? Wewe ni bazazi! Je, kuna matumizi ya mtu kama huyu? Nendeni haraka kutoka kwa macho Yangu! Kila mtu anapaswa kuwa na ueleva wazi wa Ninachosema, atiwe moyo na maneno Yangu, atambue kudura Yangu, na kujua hekima Yangu. Mara nyingi imesemwa kwamba mwili mtakatifu wa kiroho umeonekana. Hata hivyo, mnasema mwili mtakatifu wa kiroho umeonekana au la? Kile Ninachosema ni usemi mtupu? Ni nini mwili mtakatifu wa kiroho? Ni katika hali gani kuna mwili mtakatifu wa kiroho? Kwa wanadamu haiwezi kufikirika na haiwezi kueleweka. Nawaambia: Katika nafsi Yangu kuna ukamilifu, na yote ni wazi, na kila kitu ni huru (kwa sababu Nafanya kilicho cha hekima na Naongea bila kuzuiwa). Miongoni mwa mambo Mimi hufanya, hakuna ya kuaibisha, na kila kitu hufanywa katika mwanga, ili kila mtu aweze kuridhishwa kabisa. Zaidi ya hayo, hakuna anayeweza kunyakua chochote ambacho kinaweza kutumika dhidi Yangu. Haya ni maelezo ya “mtakatifu” katika mwili mtakatifu wa kiroho. Hivyo Nimesisitiza tena na tena kwamba Mimi sitaki wowote ambao hufanya vitu vya aibu, Hiki ni kitu kimoja cha amri Yangu ya utawala na pia ni sehemu moja ya tabia Yangu. “Mwili wa kiroho” unarejelea tamko Langu. Ninachosema daima kina madhumuni, daima kina hekima, lakini si chini ya udhibiti. (Mimi husema Ninachotaka kusema, na ni Roho Wangu kutamka sauti Yake na ni nafsi Yangu kuongea). Kile Ninachosema hutolewa kwa huru, na wakati hakiridhishi dhana za watu, basi huo ndio wakati wa kufichua watu. Ni mpangilio Wangu sahihi. Kwa hivyo, kila wakati ambapo mtu Niliye ananena au kutenda, daima ni nafasi nzuri kufichua kiini cha Shetani. Wakati ambapo mtu Niliye amewekwa wakfu, mwili mtakatifu wa kiroho unaibuka. Katika siku zijazo mwili mtakatifu wa kiroho hurejelea mwili, na kuna vipengele viwili kwa maana. Kuna kipengele kimoja cha maana kwa sasa, na kuna kipengele kingine cha maana baadaye. Lakini kwa siku zijazo, mwili mtakatifu wa kiroho utakuwa tofauti sana na wa sasa—utakuwa tofauti kati ya mbingu na dunia,

Hakuna anayeweza kuuelewa na itanibidi kuufichua kwenu kibinafsi.

Sura ya 95

Watu hufikiri kila kitu kuwa rahisi sana, wakati kwa kweli hali siyo hivyo. Ndani ya kila kitu kuna siri zilizofichwa, na vile vile hekima Yangu na mipango Yangu. Hakuna utondoti usioangaliwa, na yote yanapangwa na Mimi Mwenyewe. Hukumu ya siku kuu inawafikia wale wote wasionipenda kwa kweli (kumbuka, hukumu ya siku kuu inalenga kila mtu anayepokea jina hili) na kuwasababisha kulia na kusaga meno. Sauti hii ya kuomboleza hutoka jahanamu na kutoka kuzimu; si watu wanaolia, ila ni pepo. Ni hukumu Yangu inayoleta kulia huku, inayoleta wokovu wa mwisho wa mpango Wangu wa usimamizi kwa ajili ya watu. Awali Nilikuwa na matumaini kiasi kwa watu fulani. Lakini kwa kuangalia sasa, ni lazima Nitelekeze watu hawa mmoja mmoja, kwa kuwa kazi Yangu imekuja kwa hatua hii na ni kitu ambacho hakuna mtu anaweza kubadili. Wale wote ambao si wazaliwa Wangu wa kwanza au watu Wangu lazima watelekezwe na lazima waondoke hapa! Lazima muelewe kwamba, nchini China, kando na wazaliwa Wangu wa kwanza na watu Wangu, wengine wote ni watoto wa joka kubwa jekundu na wanapaswa kutupwa. Nyote mnapaswa kuelewa, hata hivyo Uchina ni taifa ambalo limelaaniwa na Mimi, na watu Wangu wachache hapo ni wale wanaotoa huduma kwa kazi Yangu ya baadaye tu. Kulisema vingine, kando na wazaliwa Wangu wa kwanza, hakuna mtu mwingine—wote wataangamizwa. Usifikiri kwamba Mimi ni wa kuzidi kiasi sana katika matendo Yangu—hii ni amri Yangu ya utawala. Wale wanaopitia laana Zangu ni walengwa wa chuki Yangu, hili ni bila shaka. Sifanyi makosa yoyote; Nikimwona mtu asiyenipendeza Nitamwondoa, na hilo linatosha kuthibitisha kwamba wewe umelaaniwa na Mimi na ni dhuria ya joka kubwa jekundu. Acha Nikufahamishe tena, kuna wazaliwa Wangu wa kwanza Uchina pekee (kando na watu Wangu wanaotoa huduma) na hii ni amri Yangu ya utawala. Lakini wazaliwa Wangu wa kwanza ni wachache sana na wote wameamuliwa kabla na Mimi—Najua ninachokifanya. Siogopi uhasi wako na Siogopi kwamba utageuka na kuniuma, kwa kuwa Nina amri Zangu za utawala na Nina ghadhabu. Yaani, Ninashikilia maafa makuu mikononi Mwangu na Siogopi chochote, kwa kuwa Nachukulia vitu vyote kuwa vimetimizwa tayari, na wakati ambapo siku hiyo itafika Nitakushughulikia kabisa. Mtu hawezi kukamilishwa au kuadilishwa na mwanadamu na kugeuka kuwa mzaliwa Wangu wa kwanza, lakini badala yake inaamuliwa kabisa na majaaliwa Yangu. Yeyote Ninayesema ni mzaliwa wa kwanza ni mzaliwa wa kwanza; usilipigania au kulinyakua. Vitu vyote vinaamuliwa na Mimi, Mungu mwenye uweza Mwenyewe.

Siku moja Nitawaruhusu nyote muone amri Zangu za utawala ni nini na ghadhabu Yangu ni nini (wote watanipigia magoti, wote wataniabudu, wote wataniomba msamaha na wote wataishi

katika utii; sasa Naruhusu tu wazaliwa Wangu wa kwanza kuona sehemu yake). Nitawafanya watoto wote wa joka kubwa jekundu waone kwamba Nimechagua wengi kutolewa kafara (isipokuwa wazaliwa Wangu wa kwanza) ili kuwakamilisha wazaliwa Wangu wa kwanza, kwamba Nimelifanya joka kubwa jekundu kuangukia hila yake ya ujanja. (Katika mpango Wangu wa usimamizi, joka kubwa jekundu linatuma wale wanaonitolea huduma—ikiwa inajumuisha kila mtu isipokuwa wazaliwa Wangu wa kwanza—kukatiza mpango Wangu wa usimamizi; lakini limeanguka katika hila yake ya ujanja lenyewe, na wote wanatoa huduma kwa kazi Yangu. Hii ni sehemu ya maana ya kweli ya Mimi kuwahamasisha wote kunitolea huduma.) Leo, wakati ambapo vitu vyote vimetimizwa, Nitawatupa wote, kuwakanyaga chini ya miguu Yangu, na kupitia hili Nitalifedhehesha joka kubwa jekundu na kulifanya liaibike kabisa (wanajaribu kudanganya kupata baraka, lakini hawakuwahi kufikiria kwamba wangenitolea huduma)—hii ni hekima Yangu. Wanaposikia hili, watu hufikiri Sina hisia au rehema, na wanafikiri kwamba Sina ubinadamu. Kwa kweli Sina hisia au rehema kwake Shetani, na aidha Mimi ni Mungu Mwenyewe anayezidi sana uwezo wa ubinadamu. Unawezaje kusema Mimi ni Mungu aliye na ubinadamu? Hujui kwamba Mimi si wa dunia hii? Hujui kwamba Niko juu ya vitu vyote? Kando na wazaliwa Wangu wa kwanza, hakuna mtu kama Mimi, hakuna mtu aliye na tabia Yangu (si tabia ya binadamu ila tabia takatifu), na hakuna mtu anayemiliki sifa Zangu.

Wakati lango la dunia ya roho linafunguliwa, mtaona siri zote, kuwawezesha kuingia kabisa katika eneo huru, kuingia katika kumbatio Langu la upendo na kuingia katika baraka Zangu za milele. Mikono Yangu imewasaidia wanadamu daima. Lakini kuna sehemu ya wanadamu ambayo Nitaokoa na sehemu ambayo Sitaokoa. (Nasema “kusaidia” kwa sababu kama Singeisaidia dunia nzima, ingeaguka imeanguka kuzimu kitambo.) Oneni hili wazi! Huu ni mpango Wangu wa usimamizi. Na mpango Wangu wa usimamizi ni nini? Niliwaumba wanadamu, lakini Sikuwahi kupanga kumpata kila mtu, ila kupata tu sehemu ndogo ya wanadamu. Kwa hivyo mbona Niliwaumba watu wengi? Nimesema awali kwamba, Nikiwepo, yote ni ufunguliwaji na uhuru, na Ninafanya chochote Ninachotaka. Nilipowaumba wanadamu, ilikuwa tu ili waishi maisha ya kawaida na kisha kungetokea sehemu ndogo ya wanadamu ambao ni wazaliwa Wangu wa kwanza, wana Wangu na watu Wangu. Inaweza kusemwa kwamba watu, mambo na vyombo vyote—kando na wazaliwa Wangu wa kwanza, watu Wangu na wana Wangu—wote ni watendaji huduma na lazima wote waangamie. Kwa njia hii mpango Wangu mzima wa usimamizi utahitimishwa. Huu ni mpango Wangu wa usimamizi, ni kazi Yangu na ni hatua Zangu zinazoendelea mbele. Wakati ambapo kila kitu kimeisha Nitakuwa mapumzikoni kabisa. Wakati huo, kila kitu kitafanywa chema na kila kitu kitafanywa kitulivu na salama.

Hatua ya kazi Yangu ni yenye kasi sana kiasi kwamba hakuna mtu anayeweza kuifikiria. Inabadilika siku kwa siku na yeyote asiyeweza kwenda kwa mwendo sawa atapata hasara; mtu

anaweza tu kushikilia mwanga mpya kila siku (ingawa amri Zangu za utawala, na maono na ukweli Ninaoshiriki havibadiliki kamwe). Kwa nini Nazungumza kila siku? Kwa nini siku zote Nakupa nuru? Je, unaelewa maana ya kweli ndani? Watu wengi bado sasa wanacheka na kufanya mzaha na hawawezi kuwa makini. Hawazingatii maneno Yangu kabisa, lakini wanahisi tu wasiwasi wa muda wanapoyasikia. Baadaye, maneno Yangu yanasahaulika punde na punde hawajui utambulisho wao wenyewe na wanakuwa wazembe. Je, unajua hadhi yako ni ipi? Iwapo mtu ananitolea huduma au anajaaliwa na kuchaguliwa na Mimi kunasimamiwa na mikono Yangu tu na hakuna mtu anayeweza kubadili hili—ni lazima Nifanye hili Mwenyewe, lazima Niwachague na kuwajaalia Mimi Mwenyewe. Nani anathubutu kusema Mimi ni Mungu asiye na hekima? Kila neno Ninalosema na kila kitu Ninachofanya ni hekima Yangu. Nani anathubutu kukatiza usimamizi Wangu tena au kuharibu mipango Yangu? Bila shaka Sitamsamehe! Wakati uko mikononi Mwangu na Siogopi kucheleweshwa; Mimi siye Yule anayeamua wakati ambao mpango Wangu wa usimamizi utaisha? Hauamuliwi na wazo Langu moja tu? Ninaposema umeisha, umeisha, na unaisha Ninaposema uishe. Sina haraka na Nitafanya mipango ya kufaa. Mwanadamu lazima asiingilie kazi Yangu na ni lazima asinifanyie mambo kama apendavyo. Namlaani yeyote anayeingilia—hii ni mojawapo ya amri Zangu za utawala. Mimi Mwenyewe nafanya kazi Yangu na Simhitaji yeyote mwingine (Naruhusu wale watendaji huduma kutenda, vinginevyo hawangethubutu kutenda kwa haraka au bila kufikiri). Kazi yote inapangwa na Mimi, inaamuliwa na Mimi, kwa kuwa Mimi ndiye Mungu mmoja Mwenyewe.

Mataifa yote ya dunia yanapigana kwa ajili ya mamlaka na faida na kupigania ardhi, lakini usishtuke, vitu hivi vyote vinanihudumia. Na kwa nini Nasema vinanihudumia? Nafanya vitu bila jitihada. Kumhukumu Shetani kwanza Nawafanya wagombane miongoni mwao wenyewe na mwishowe kuwaleta kwa uangamizi na kuwafanya waanguke katika hila zao za ujanja (wanataka kupigana na Mimi kwa ajili ya mamlaka, lakini wanaishia kunihudumia). Nazungumza tu na kutoa maagizo Yangu na kila mtu atafanya kile Nitakachokwambia ufanye, au vinginevyo Nitakuangamiza mara moja. Vitu hivi vyote ni sehemu ya hukumu Yangu, kwa kuwa Naamuru vitu vyote, na vitu vyote vinaagizwa na Mimi. Yeyote anayefanya chochote anafanya hivyo pasipo kutaka, kufanya hivyo kwa mpango Wangu mwenyewe, na Natumai kwamba mnaweza kujaa hekima Yangu katika matukio ambayo yatafika karibuni. Msichukue mtazamo usio mwangalifu, ila mnikaribie zaidi mara nyingi wakati mambo yanapowafika; kuweni makini na kujihadhari zaidi katika mambo yote kuepuka kukosea kuadibu Kwangu, na kuepuka kuwa windo la ujanja za Shetani. Mnapaswa kupata umaizi kutoka kwa maneno Yangu, mjue kile Nilicho, na kuona kile Ninacho. Ni lazima mfanye vitu kulingana na mitazamo Yangu ya maana na lazima msitende bila uangalifu. Fanyeni kile Ninachofanya, na msemi kile Ninachokisema. Nasema vitu hivi kwenu mapema ili mweze kuepuka kufanya makosa na kuepuka kujaribiwa. Na

kile Nilicho na Ninacho ni nini? Kweli mnajua? Uchungu Ninaoupitia ni sehemu ya kile Nilicho, kwa kuwa ni sehemu ya ubinadamu Wangu wa kawaida, na kile Nilicho kinaweza kupatikana pia katika uungu Wangu kamili—mnajua hili? Kile Nilicho kinajumuishwa na vipengele viwili: Kipengele kimoja ni kile cha ubinadamu Wangu, ilhali kingine ni kile cha uungu Wangu kamili. Ni vipengele hivi viwili tu vikijumuishwa pamoja ndivyo vinamuunda Mungu Mwenyewe kamili. Kile ambacho uungu Wangu kamili ndicho pia kinajumuisha mambo mengi: Sizuiliwi na mtu, suala au jambo lolote; Navuka mipaka ya mazingira yote; Nimezidi mipaka ya wakati au nafasi au jiografia; Najua watu, masuala na vitu vyote kweli kama kiganja cha mkono Wangu; na bado Mimi ni nyama na mifupa, katika umbo linalogusika; Mimi bado ni mtu huyu machoni pa watu, lakini asili imebadilika—si nyama, ila ni mwili. Vitu hivi ni sehemu yake ndogo tu. Wazaliwa Wangu wa kwanza wote watakuwa hivi pia katika siku za baadaye; hii ni njia ambayo lazima itembelewe, na wale ambao wamehukumiwa hawawezi kuepuka. Ninapokuwa nikifanya hili, wale wote ambao hawajajaaliwa watafukuzwa wote (kwa kuwa huku ni Shetani kunijaribu kuona kama maneno Yangu ni sahihi). Wale ambao wamejaaliwa hawawezi kulitoroka bila kujali wanapokwenda, na mtaona humo kanuni za hili tendo Langu. Kile Ninacho kinarejelea maarifa Yangu, hekima Yangu, werevu Wangu na kila neno Ninalosema. Ubinadamu Wangu na uungu Wangu unakimiliki. Yaani, yote ambayo yanafanywa na ubinadamu Wangu na vile vile kile ambacho kinafanywa na uungu Wangu ni kile Ninacho; hakuna anayeweza kuchukua vitu hivi au kuviondoa, Navimiliki, na hakuna anayeweza kuvibadili. Hii ndiyo amri Yangu ya utawala kali zaidi (kwani katika dhana za mwanadamu, vitu vingi Ninavyovifanya havipatani na dhana zao na haviwezi kueleweka na mwanadamu; hii ndiyo amri ambayo kila mtu huikosea kwa urahisi zaidi na pia ndiyo kali zaidi, kwa hivyo maisha yao humo lazima yapoteze). Nitasema tena, ni lazima mchukue mtazamo wa uangalifu sana kwa kile Ninachowasihi kufanya—ni lazima msiwe wazembe!

Sura ya 96

Nitamwadibu kila mtu aliyezaliwa kutoka Kwangu ambaye bado hanijui ili kuonyesha ghadhabu Yangu yote, kuonyesha nguvu Zangu kuu, na kuonyesha hekima Yangu kamili. Ndani Yangu kila kitu ni chenye haki na bila shaka hakuna udhalimu, hakuna udanganyifu, na hakuna upotovu; yeyote ambaye ni mpotovu na mdanganyifu lazima awe ni mwana wa jahanamu—lazima amezaliwa huko kuzimu. Ndani Yangu kila kitu ni cha wazi; chochote Ninachosema kukamilisha kinakamilika na chochote Ninachosema kuanzisha kinaanzishwa, na hakuna mtu anayeweza kubadilisha au kuiga mambo haya kwa sababu Mimi ndimi Mungu Mwenyewe wa pekee. Katika kinachokaribia kuja, kila mtu aliye katika kikundi cha wazaliwa Wangu wa kwanza walioamuliwa kabla na walioteuliwa watafichuliwa mmoja baada ya mwingine, na yeyote asiye katika kikundi cha wazaliwa wa kwanza ataondolewa na Mimi kupitia kwa hili.

Hivi ndivyo Ninavyofanya na kukamilisha kazi Yangu. Hivi sasa, Ninawafunua watu wengine ili tu kwamba wazaliwa Wangu wa kwanza waweze kuona matendo Yangu ya ajabu, lakini baadaye Sitafanya kazi kwa njia hii. Badala yake, Nitaendelea kutoka kwa hali ya kawaida badala ya kuwaacha waonyeshe hali zao za kweli mmoja baada ya mwingine (kwa sababu kimsingi mapepo wote ni sawa, inatosha tu kuchagua wachache kama vithibitisho). Wazaliwa Wangu wa kwanza wote wanaelewa vyema, na hakuna haja ya Mimi kufafanua (kwa sababu katika wakati uliowekwa, hakika wao watafichuliwa mmoja baada ya mwingine).

Ni tabia Yangu kutimiza ahadi Zangu, na ndani Yangu hakuna kitu kilichofichwa au kilichofichika. Nitawaambia kila kitu kuhusu kila mojawapo ya vitu ambavyo mnapaswa kuelewa, na Sitawaambia kabisa kuhusu kitu chochote msichopaswa kujua, msije mkakosa kusimama imara. Msishikilie vitu vidogo vidogo na hapo mpoteze mambo muhimu—hakika hiyo haina thamani kabisa. Amini kwamba Mimi ni mwenyezi Mungu na kila kitu kitafanikishwa na vyote vitakuwa rahisi na vya kupendeza. Hivi ndivyo Ninavyofanya mambo. Yeyote anayeamini, Ninamruhusu aone, na yeyote asiyeamini, Simruhusu kujua na Simruhusu aelewe kamwe. Ndani Yangu hakuna hisia au rehema, na yeyote anayekosea kuadibu Kwangu hakika Nitamuua bila kumhurumia, Nikiwatendea wote sawa. Mimi niko sawa kwa kila mtu—Sina hisia za kibinafsi nami Sitendi kwa kuonyesha hisia hata kidogo. Je, watu wanawezaje kukosa kuona haki na uadhama Wangu kupitia katika hili? Hii ni hekima Yangu na tabia Yangu, ambayo hakuna mtu anayeweza kubadilisha na hakuna mtu anayeweza kujua kabisa. Daima mikono Yangu inadhibiti kila kitu, wakati wote, na Mimi hupanga kila kitu kunihudumia kwa amri Yangu wakati wowote. Watu wengi wanatoa huduma kwa niaba Yangu ili kutimiza mpango Wangu wa usimamizi, lakini hatimaye wanaziona baraka lakini hawawezi kuzifurahia—ni ya kusikitisha jinsi gani! Lakini hakuna mtu anayeweza kuubadilisha moyo Wangu. Hii ni amri Yangu ya utawala (inapokuja kwa amri ya utawala, hiyo ndiyo hakuna mtu anayeweza kubadilisha, hivyo Ninapozungumzia wakati ujao, kama Nimepania kitu, hakika hiyo ni amri Yangu ya utawala. Kumbuka! Usifanye makosa dhidi ya hili, usije ukapoteza), na pia ni sehemu ya mpango Wangu wa usimamizi. Ni kazi Yangu mwenyewe, si kitu tu ambacho mtu yeyote anaweza kufanya. Lazima Nifanye jambo hili—ni lazima Nipange hili, ambayo inatosha kuonyesha kudura Yangu na kudhihirisha ghadhabu Yangu.

Watu wengi bado hawajui na hawaelewi kuhusu ubinadamu Wangu. Nimesema mara kadhaa, lakini ninyi bado hamna uhakika na hamwelewi sana. Lakini hii ni kazi Yangu, na sasa, wakati huu, yeyote anayejua, anajua, na yeyote asiyejua, Simshawishi. Inaweza tu kuwa namna hii. Nimezungumza waziwazi na Sitasema baadaye (kwa sababu Nimesema mengi sana, na Nimeyasema wazi sana. Mtu ambaye ananijua hakika ana kazi ya Roho Mtakatifu na bila shaka ni mmoja wa wazaliwa Wangu wa kwanza. Mtu ambaye hanijui amefanya uamuzi kutonijua,

ikithibitisha kwamba Nimeshaondoa Roho Wangu kutoka kwake). Lakini mwishowe, Nitamfanya kila mtu anijue—anijue kabisa katika ubinadamu Wangu na katika utakatifu Wangu. Hizi ni hatua za kazi Yangu, na lazima Nifanye kazi kwa njia hii. Hii pia ni amri Yangu ya utawala. Lazima kila mtu aniite Mimi Mungu pekee wa kweli, na kunisifu na kunihimidi bila kukoma.

Mpango Wangu wa usimamizi umekwisha kukamilishwa kabisa, na kila kitu kimefanikishwa kitambo. Kwa macho ya binadamu inaonekana kana kwamba kazi Yangu nyingi bado inaendelea, lakini tayari Nimeipanga vizuri na yote ambayo yanatarajiwa ni ukamilisho wake kwa kulingana na hatua Zangu kazi moja baada ya nyingine (hii ni kwa sababu kabla ya uumbaji wa ulimwengu Nilishajaalia ni nani anaweza kusimama imara katika majaribu, nani hawezi kuteuliwa na kuamuliwa kabla na Mimi, na nani hawezi kushiriki katika mateso Yangu. Wale ambao wanaweza kushiriki katika mateso Yangu—yaani, wale walioamuliwa kabla na kuteuliwa na Mimi, hakika Nitawahifadhi na kuwawezesha kuvuka mipaka ya kila kitu). Niko dhahiri moyoni Mwangu kuhusu nani aliye katika kila jukumu. Najua vema ni nani anayetoa huduma Kwangu, ni nani mzaliwa wa kwanza, na ni nani aliye kati ya wana Wangu na watu Wangu. Najua jambo hili kama kiganja cha mkono Wangu. Mtu yeyote Niliyesema zamani kuwa ni mzaliwa wa kwanza bado ni mzaliwa wa kwanza sasa, na yeyote Niliyesema zamani kuwa si mzaliwa wa kwanza bado si mzaliwa wa kwanza sasa. Chochote Ninachokifanya, Sijuti, na Sikibadilishi kwa urahisi. Namaanisha kile Ninachosema (ndani Yangu hakuna chochote kisicho na maana), na hakibadiliki kamwe! Wale ambao wanatoa huduma Kwangu daima hutoa huduma Kwangu: Wao ni ng'ombe Wangu; wao ni farasi Wangu (lakini watu hawa hawajawahi kupata nuru katika roho zao, Ninapowatumia wao huwa muhimu, lakini wakati Siwatumii Ninawaua. Ninapozungumza kuhusu ng'ombe na farasi, Ninamaanisha wale ambao hawajapata nuru katika roho zao, ambao hawanijui, na ambao wananiasi, na hata kama wao ni watiifu na wanyenyekevu na wepesi na waaminifu, wao bado ni ng'ombe na farasi halisi). Sasa, watu wengi ni watukutu na hawajafunguliwa mbele Yangu, wakiongea na kucheka kwa fujo, wakitenda kwa namna isiyo ya heshima—wanaona tu ubinadamu Wangu, na sio uungu Wangu. Katika ubinadamu Wangu tabia hizi zinaweza kukubaliwa bila lawama na Niweze kuzisamehe, lakini katika uungu Wangu si rahisi sana. Katika siku zijazo Nitaamua kwamba wewe umetenda dhambi kwa kunikufuru. Kwa maneno mengine, ubinadamu Wangu unaweza kukosewa, lakini uungu Wangu hauwezi, na yeyote anayepingana na Mimi kidogo, Nitamhukumu mara moja, bila kuchelewa. Usifikiri kuwa kwa sababu umeshirikiana kwa miaka mingi na mtu huyu Niliye na umejuana na Mimi, unaweza kuzungumza na kutenda kwa utukutu. Kwa kweli Sijali sana! Haijalishi ni nani, Nitamtendea kwa haki. Hii ni haki Yangu.

Siri Zangu zinafichuliwa kwa watu kila siku, nazo huwa wazi zaidi kila siku, zikifuata hatua

za ufunuo, ambayo inatosha kuonyesha kasi ya kazi Yangu. Hii ni hekima Yangu (Siisemi moja kwa moja. Ninawapa nuru wazaliwa Wangu wa kwanza na kuwapofusha watoto wa joka kuu jekundu). Zaidi ya hayo, leo Nitawafichulia siri Yangu kupitia kwa mwanangu. Mambo ambayo hayafikiriki na watu Nitawafichulia leo ili kuwawezesha kujua kabisa na muwe na ufahamu dhahiri. Zaidi ya hayo, siri hii ipo ndani ya kila mtu nje ya wazaliwa Wangu wa kwanza, lakini hakuna mtu anayeweza kuielewa. Ingawa imo ndani ya kila mtu, hakuna mtu anayeweza kuitambua. Ninasema nini? Katika kazi Yangu wakati huu na katika matamshi Yangu wakati huu, mara nyingi Mimi hutaja joka kuu jekundu, Shetani, ibilisi, na malaika mkuu. Wao ni nini? Je, uhusiano wao ni nini? Ni nini kinachojidhihirisha katika mambo haya? Udhihirisho wa joka kuu jekundu ni upinzani Kwangu, ukosefu wa ufahamu na utambuzi wa maana ya maneno Yangu, mateso ya mara kwa mara Kwangu, na kutafuta kutumia njama ili kuzuia usimamizi Wangu. Shetani anadhihirika kama ifuatavyo: kupambania mamlaka na Mimi, kutaka kuwamiliki watu Wangu wateule, na kutoa maneno hasi ili kuwadanganya watu Wangu. Udhihirisho wa ibilisi (wale ambao hawalikubali jina Langu, ambao hawaamini, wote ni mapepo) ni kama ifuatavyo: kupenda raha za mwili, kujiingiza katika tamaa mbaya, kuishi chini ya utumwa wa Shetani, wengine kupinga na wengine kuniunga mkono (lakini kutothibitisha kwamba wao ni wana Wangu wapendwa). Udhihirisho wa malaika mkuu ni kama ifuatavyo: kuzungumza kwa kiburi, kuwa asiyemcha Mungu, mara nyingi kuchukua sauti Yangu kuwahubiria watu, kuzingatia tu kuniiga kwa nje, kula kile Ninachokula na kutumia kile Ninachotumia; kwa ufupi, kutaka kuwa sawa na Mimi, kuwa mwenye tamaa ya makuu lakini kukosa ubora Wangu na kutokuwa na maisha Yangu, kuwa bure. Shetani, ibilisi, na malaika mkuu ni maonyesho ya mfano hasa wa joka kuu jekundu, kwa hiyo wale ambao hawajaamuliwa kabla na kuchaguliwa na Mimi wote ni watoto wa joka kuu jekundu: Hiyo ni hivyo kabisa! Hawa wote ni adui Zangu. (Hata hivyo mivurugo ya Shetani haihusishwi. Ikiwa asili yako ni ubora Wangu, hakuna mtu anayeweza kuibadilisha. Kwa sababu sasa bado unaishi katika mwili, mara kwa mara utakabiliwa na majaribu ya Shetani—hii haiwezi kuepukika—lakini lazima daima uwe makini.) Kwa hiyo, Nitawaacha watoto wote wa joka kuu jekundu nje ya wazaliwa Wangu wa kwanza. Asili yao haiwezi kubadilika daima, nao ni ubora wa Shetani. Ni ibilisi wanayemdhihirisha, na ni malaika mkuu wanayeishi kwa kumdhihirisha. Hii ni kweli kabisa. Joka kuu jekundu Ninayezungumzia si joka kuu jekundu lolote fulani; badala yake ni pepo mbaya anayenipinga Mimi, ambaye kwaye “joka kuu jekundu” ni kisawe. Hivyo roho zote nje ya Roho Mtakatifu ni roho mbaya, na zinaweza pia kusemwa kuwa ni watoto wa joka kuu jekundu. Haya yote yanapaswa kuwa wazi kabisa kwa kila mtu.

Sura ya 97

Nitafanya kila mtu aone matendo Yangu ya ajabu na kusikia maneno Yangu ya hekima. Ni

lazima iwe kila mtu na ni lazima iwe juu ya kila suala. Hii ni amri Yangu ya utawala na ni ghadhabu Yangu. Nitahusisha kila mtu na kila jambo ili watu wote kutoka mwisho mmoja wa ulimwengu hadi mwingine wataona kwa macho yao wenyewe, la sivyo Sitaacha kamwe. Ghadhabu Yangu imemwagwa kikamilifu na hakuna hata chembe imezuiwa. Inaelekezwa kwa kila mtu mmoja ambaye anakubali jina hili (hivi karibuni itageuzwa juu ya mataifa yote ya dunia). Na ghadhabu Yangu ni nini? Ni kali kiasi gani? Je, ghadhabu Yangu inamwangukia mtu wa aina gani? Watu wengi wanafikiri kuwa ghadhabu ni hasira kali kabisa, lakini hii haiielezi kikamilifu. Ghadhabu Yangu na amri Zangu za utawala ni sehemu mbili zisizotenganishwa; Ninapozifanya amri Zangu za utawala kuwa sheria, ghadhabu hufuata nyuma yake. Kwa hiyo ghadhabu ni nini? Ghadhabu ni kiwango cha hukumu Ninachotoa kwa watu na ni kanuni ya kufanywa kuwa sheria kwa amri Yangu yoyote ya utawala. Yeyote anayekosea mojawapo ya amri Zangu, ghadhabu Yangu itakuwa kulingana na kiwango chake, kulingana na amri ambayo imekosewa. Pamoja na ghadhabu huja amri Zangu za utawala, na pamoja na amri Zangu za utawala huja ghadhabu. Amri Zangu za utawala na ghadhabu hufanya uzima usiotenganishwa. Ni hukumu kali zaidi na hakuna mtu anayeweza kuikosea. Watu wote wanapaswa kuizingatia, la sivyo wataona vigumu kuepuka kupigwa chini na mkono Wangu. Watu hawakuwahi kujifunza jambo hilo katika enzi zote (ingawa watu wengine waliteseka machungu yaliyosababishwa na maafa makubwa, bado hawakutambua kulihusu; lakini hili hasa linaanza kufanywa kuwa sheria sasa), lakini leo ninawafichulia yote, ili muweze kuepuka kusababisha kosa.

Watu wote wanapaswa kusikia sauti Yangu na kuamini maneno Yangu, vinginevyo Sitatenda lolote wala kufanya kazi yoyote. Maneno Yangu yote na matendo ni mifano ambayo mnapaswa kufuata; hayo ni mifano yenu bora na hayo ni mifano ya ninyi kufuata. Sababu ya Mimi kuwa mwili ni kwamba muweze kuona kile Nilicho na nilicho nacho katika ubinadamu Wangu. Katika siku zijazo, Nitawaruhusu kushuhudia kile Nilicho na nilicho Nacho katika uungu Wangu. Mambo lazima yaende hatua kwa hatua kwa njia hii. Vinginevyo, watu hawataweza kuamini kabisa, na hawatakuwa na ujuzi kunihusu. Badala yake watakuwa tu bila uwazi na kutoweza kutofautisha kuhusu maono na hawataweza kuwa na ufahamu wa wazi wa Mimi. Maneno Yangu yameonyesha kuwa nafsi Yangu imeonekana kwenu kabisa, watu tu ndio wapumbavu na wasiojua, kwa hiyo wanasikia maneno Yangu na bado hawanijui Mimi. Watu bado wananikataa Mimi kama kupata mwili kwa sasa, kwa hiyo Ninatumia ghadhabu Yangu na amri Zangu za utawala ili kuadhibu enzi hii ya zamani mbovu na ya uasherati na kumwaibisha Shetani na ibilisi kabisa. Hii ndiyo njia pekee, ni hatima ya wanadamu, na ni mwisho ambao unawasubiri wanadamu. Matokeo yake ni hitimisho lililopita kwamba hakuna mtu anayeweza kubadilisha au kujitetea asamehewe. Mimi tu ndiye Nina uamuzi wa mwisho; huu ni usimamizi Wangu na ni mpango Wangu. Watu wote wanapaswa kuamini na kushawishika katika moyo na

kwa neno. Wale ambao wanapata bahati nzuri katika maisha haya bila shaka watateseka milele yote, huku wale wanaoteseka katika maisha haya hakika watabarikiwa katika milele yote—hii Nimeiamua kabla na hakuna mtu anayeweza kuibadilisha. Hakuna mtu anayeweza kubadili moyo Wangu na hakuna mtu anayeweza kuongeza hata neno moja zaidi kwa maneno Yangu, sembuse wao kuruhusiwa kuondoa neno lolote kiholela; hakika Nitawaadibu wakosaji wote.

Mafumbo Yangu yanafichuliwa kwenu kila siku—je, mnayaelewa kweli? Je, mna hakika kuyahusu? Je, unaweza kung'amua wakati Shetani anakudanganya? Hii inaamuliwa kwa mujibu wa vimo vyenu katika maisha. Kwa kuwa Ninasema kwamba vitu vyote vimeamuliwa kabla na Mimi, kwa nini basi ninapata mwili mimi binafsi kuwakamilisha wanangu wazaliwa wa kwanza? Zaidi ya hayo, kwa nini nimefanya kazi nyingi sana ambazo watu wanazifikiria kama zisizo na maana? Je, ni Mimi Niliyechanganyikiwa? Kumbuka hili! Kila kitu Ninachofanya hakifanyiki tu ili kuwapata wana Wangu wazaliwa wa kwanza lakini la muhimu zaidi vinafanywa kumwaibisha Shetani. Ingawa ananikiuka, bado Nina uwezo wa kuwafanya wazawa wake waasi dhidi yake, na kugeuka kunisifu. Aidha, kila Ninachofana ni ili hatua ifuatayo ya kazi itaendelea vizuri, na kwamba ulimwengu wote utafurahi na kunisifu na vitu vyote vinavyopumua vitanipigia goti na kunitukuza; hiyo kweli itakuwa siku ya utukufu. Ninashikilia vitu vyote mikononi Mwangu na wakati radi saba zitakapozuka vitu vyote vitakuwa vimekamilishwa kabisa, visibadilike kamwe, vyote vimetengenezwa. Kutoka wakati huo kuendelea maisha mapya ya mbingu na nchi mpya yataingiwa, kuingia katika hali mpya kabisa, na maisha ya ufalme yataanza. Lakini hali ni vipi ndani ya ufalme? Watu hawawezi kuelewa wazi kabisa (kwa sababu hakuna mtu aliyewahi kuonja maisha ya ufalme kabla, na hivyo yamefikiriwa tu katika akili za watu na kufikiriwa ndani ya mioyo yao). Katika kugeuka kutoka kwa maisha ya kanisa hadi kwa maisha ya ufalme, ambayo ni kugeuka kutoka hali ya sasa hadi hali ya baadaye, mambo mengi yatatokea wakati huu ambayo watu hawajawahi kufikiria awali. Maisha ya Kanisa ni utangulizi wa uingiaji katika maisha ya ufalme, hivyo kabla ya maisha ya ufalme kutokea Sitaacha jitihada yoyote katika kuendeleza maisha ya kanisa. Maisha ya kanisa ni nini? Ni kila mtu, ikiwa ni pamoja na wanangu wazaliwa wa kwanza, akila, kunywa na kufurahia maneno Yangu na kunijua, hivyo kupokea uchomaji na utakaso Wangu, ili kuelewa amri Zangu za utawala, hukumu Yangu na ghadhabu Yangu, ili aweze kuepuka kusababisha kosa katika maisha ya ufalme. Na maisha ya ufalme ni nini? Maisha ya Ufalme ni pale ambapo wanangu wazaliwa wa kwanza wanaanza kutawala kama wafalme pamoja na Mimi, wakitawala watu wote na mataifa yote (wanangu wazaliwa wa kwanza na Mimi tu ndio tunaweza kufurahia maisha ya ufalme). Ingawa wana Wangu na watu Wangu kutoka kwa watu wote na mataifa yote wataingia katika ufalme, hawawezi kufurahia maisha ya ufalme. Uzima wa ufalme unaweza kufurahiwa tu na wale wanaoingia katika ulimwengu wa kiroho. Hivyo ni wanangu wazaliwa wa kwanza tu na Mimi

tunaoweza kuishi katika mwili, wakati wana wangu na watu wangu wanaendelea kuishi katika mwili. (Lakini huu sio mwili ambao umepotoshwa na Shetani. Huu ni umuhimu wa wana Wangu wazaliwa wa kwanza kutawala pamoja nami kama wafalme.) Roho za watu wengine wote zitachukuliwa, roho na miili itachukuliwa na kutupwa Kuzimuni. Hiyo ni kusema kuwa watu hawa wataangamia kabisa na watakoma kuwepo (na bado wanapaswa kupitia katika utumwa wote na ukatili wa Shetani, kama vile shida na maafa). Mara hii itakapofanyika, maisha ya ufalme yatakuwa kwenye njia sahihi, na Nitaanza kufichua matendo Yangu rasmi (kufichuliwa waziwazi na sio kufichwa). Kutoka wakati huo kuendelea, hakika hakutakuwa na kutanafusi tena na machozi. (Kwa maana hakutakuwa na kitu chochote ambacho kinaweza kuwaumiza watu, au kuwafanya kulia au kuwasababishia mateso, na hii inahusu wana Wangu na watu Wangu pia; lakini kuna jambo moja ambalo linastahili kusesitizwa, ambalo ni kwamba wana Wangu na watu Wangu watakuwa miili milele.) Wote watakuwa wenye furaha na kuonekana wenye furaha. Hakitakuwa kitu chochote cha kimwili, kitakuwa kitu ambacho hakiwezi kuonekana kwa macho ya kimwili. Wale ambao ni wanangu wazaliwa wa kwanza watakuwa na uwezo wa kufurahia pia; hili ni tendo Langu la ajabu na mamlaka Yangu.

Ninatamani kwamba ninyi muwe na uwezo wa kutafuta mapenzi Yangu na muuhurumie moyo Wangu wakati wote. Raha isiyodumu inaweza kuharibu maisha yako yote, wakati mateso ya muda mfupi yanaweza kukaribisha baraka ya milele. Usiwe mwenye huzuni; hii ndiyo njia ambayo lazima itembewe. Nimesema mara nyingi kabla: “Kwa wale wanaotumia rasilimali kwa dhati kwa ajili Yangu, hakika Nitakubariki sana.” Baraka ni nini? Siyo tu zile zinazopatikana leo, lakini zaidi ya hayo ni zile zitakazofurahiwa katika siku zijazo—hizi tu ndizo baraka za kweli. Mnaporudi katika Mlima Sayuni, mtaonyesha shukrani isiyo na mwisho kwa mateso yenu ya sasa, kwa maana hii ni baraka Yangu. Kuishi sasa katika mwili ni kuwa juu ya Mlima Sayuni (kumaanisha ya kuwa unaishi ndani Yangu), wakati kuishi katika mwili kesho kutakuwa siku ya utukufu, na hii hata zaidi ni kuwa juu ya Mlima Sayuni. Baada ya kusikia maneno haya Ninayosema, kisha mnaelewa maana ya Mlima Sayuni. Mlima Sayuni ni kisawe cha ufalme, na pia ni ulimwengu wa kiroho. Katika Mlima Sayuni wa leo, ninyi mko katika mwili mkipata faraja na kupata neema Yangu; juu ya Mlima Sayuni wa siku zijazo, mtakuwa katika mwili mkifurahia baraka ya kutawala kama wafalme. Hii lazima bila shaka isipuuzwe. Na msiruhusu nyakati ambapo baraka zinaweza kupatikana zipite hata kidogo; leo ni leo, hata hivyo, na ni tofauti sana na kesho. Unapokuja kufurahia baraka, utafikiri kuwa neema ya leo haistahili kutajwa. Hili ndilo Ninalokuaminia, na ni ushauri Wangu wa mwisho.

Sura ya 98

Mambo yote yatakuja juu ya kila mmoja wenu, na yatawawezesha kujua zaidi juu Yangu na

kuwa na uhakika zaidi juu Yangu. Yatawawezesha kunijua, Mungu mmoja Mwenyewe, kunijua Mimi Mwenye uweza, kunijua Mimi Mungu Mwenyewe mwenye mwili. Baadaye, Nitatoka katika mwili, Nirudi Sayuni, Nirudi katika nchi nzuri ya Kanaani, ambayo ni makazi Yangu, ndiyo hatima Yangu, na ndio msingi ambao niliumba vitu vyote. Sasa hakuna yeyote kati yenu anayeelewa maana ya maneno ambayo Ninasema, hakuna mtu hata mmoja ambaye anaweza kuelewa maana ya maneno haya. Ni wakati tu kila kitu kitafichuliwa kwenu ndipo mtaelewa kwa nini Ninasema maneno haya. Mimi si wa ulimwengu na Mimi sio hata wa ulimwengu kwa sababu Mimi ni Mungu Mwenyewe wa pekee. Ninashikilia ulimwengu dunia wote mkononi Mwangu, Mimi Mwenyewe Ninatawala, na watu wanaweza tu kutii mamlaka Yangu, kulitaja jina Langu takatifu, kunishangilia na kunisifu. Kila kitu kitafunuliwa kwenu hatua kwa hatua. Ingawa hakuna kitu kilichofichwa, ninyi bado hamwezi kuelewa njia Yangu ya kuzungumza, na sauti ya maneno Yangu. Bado hamwelewi mpango Wangu wa usimamizi unahusu nini. Kwa hiyo, Nitawaambia baadaye kuhusu mambo yote ambayo hamwelewi kwa yale Niliyoyasema kwa sababu, Kwangu Mimi, kila kitu ni rahisi na wazi wakati, kwenu, ni vigumu sana, hamwelewi tu kabisa. Kwa hiyo, Nitabadili njia Yangu ya kuzungumza, Sitaunganisha mambo pamoja Ninaponena lakini Nitafafanua kila hoja moja baada ya nyingine.

Kufufuka kutoka kwa wafu kunahusu nini? Je, ni kufa katika mwili na kisha kurudi kwenye mwili baada ya kifo? Je, huku kunaitwa kufufuka kutoka kwa wafu? Je, ni rahisi vile? Mimi ni mwenyezi Mungu, unajua nini kuhusu hili? Je, mnaelewaje hili? Je, kufufuka kutoka kwa wafu wakati wa kupata Kwangu mwili mara ya kwanza kwa kweli kunaweza kuchukuliwa neno kwa neno? Je, mchakato huo ulikuwa kama ulivyoelezwa katika maandiko? Nimesema kuwa kama Sizungumzi kwa uwazi, kama Sielezi wazi, hakuna mtu atakayeweza kuelewa maana ya maneno Yangu. Hakuna mtu hata mmoja katika enzi zote ambaye hakufikiri kwamba kufufuka kutoka kwa wafu kulikuwa vile. Tangu uumbaji wa dunia hakuna mtu aliyeelewa maana halisi ya hili. Je, nilipigwa misumari msalabani kwa kweli? Na, baada ya kifo, je, nilitoka kaburini? Ilikuwa namna hii kwa kweli? Je, hili linaezekana kweli? Hakuna mtu katika enzi zote ambaye ameweka jitihada yoyote katika hili, hakuna mtu ambaye amenijua kutoka kwa hili na hakuna mtu hata mmoja ambaye haamini, kila mtu anadhani kuwa hili ni kweli. Hawajui kwamba kila neno Langu lina maana ya ndani. Basi, kufufuka kutoka kwa wafu ni nini hasa? (Hivi karibuni, mtapitia jambo hili, kwa hivyo Nitawaambia kuhusu hilo mapema.) Kila kiumbe aliyeumbwa anataka kuishi kuliko kufa. Kutoka kwa mtazamo Wangu, kifo cha mwili sio kifo halisi. Wakati Roho Wangu anarudishwa kutoka kwa mtu, mtu huyo hufa. Kwa hiyo, Ninawaita wale mapepo wote waliopotoshwa na Shetani (wale ambao hawana imani, wasioamini wote) wafu. Tangu kuumbwa kwa dunia, Nimeongeza Roho Wangu kwa kila mtu Niliyemchagua. Hata hivyo, baada ya awamu iliyofuatia uumbaji, watu walimilikiwa na Shetani kwa kipindi cha muda. Kwa

hiyo Niliondoka na watu wakaanza kuteseka (mateso Niliyovumilia Nilipopata mwili na kusulubishwa msalabani, kama ilivyoelezwa). Hata hivyo, kwa wakati uliopangiwa kabla na Mimi (wakati ambapo kuwaacha Kwangu watu kulimalizika), Niliwarejesha Kwangu watu Niliowaamulia kabla na Nikaweka tena Roho Wangu ndani yenu ili mpate kufufuka. Hii inaitwa “kufufuka kutoka kwa wafu.” Sasa, wale wanaoishi kwa kweli katika Roho Wangu wote wameshashinda uwezo wa binadamu, na wote wanaishi katika mwili. Hata hivyo, kabla ya muda mrefu, ninyi nyote mtaondoa fikira zenu, mtupe mawazo yenu, na kutupa mtego wote wa kidunia. Lakini, siyo, kama watu wanavyofikiria, kufufuka kutoka kwa wafu baada ya mateso. Kwamba ninyi mnaishi sasa ni sharti la awali la kuishi katika mwili, ni njia muhimu ya kuingia katika ulimwengu wa kiroho. Kuzidi uwezo wa ubinadamu wa kawaida Ninaozungumza kuhusu kunamaanisha kutokuwa na familia, kutokuwa na mke, kutokuwa na watoto na mahitaji ya kibinadamu. Ni kuzingatia tu kuishi kwa kudhihirisha mfano Wangu, kuzingatia tu kuingia ndani Yangu na kutofikiria juu ya mambo mengine nje Yangu. Mahali popote unapoenda ni nyumbani kwako, huku ni kuvuka mipaka kwa ubinadamu wa kawaida. Ninyi mmelewa visivyo kabisa maneno haya Yangu, ufahamu wenu ni wa kina kifupi sana. Je, Nitaonekanaje kwa mataifa yote na watu wote? Katika mwili leo? Hapana! Wakati utakapokuja, Nitaonekana katika mwili Wangu katika kila taifa la ulimwengu. Wakati ambapo wageni wanawahitaji muwachunge bado haujafika. Wakati huo ninyi mtahitaji kuja nje ya mwili na kuingia katika mwili ili muwalishe. Huu ni ukweli lakini sio “kufufuka kutoka kwa wafu” ambao watu wanafikiria. Wakati uliowekwa, mtatoka katika mwili bila kujua na kuingia katika ulimwengu wa kiroho na kutawala mataifa yote pamoja nami. Wakati haujafika bado. Ninapowahitaji kuwa katika mwili mtakuwa katika mwili (kulingana na mahitaji ya kazi Yangu, ninyi lazima muwe na fikira sasa, bado lazima muishi katika mwili, hivyo mnapaswa bado kufanya mambo ambayo mnapaswa kufanya katika mwili kulingana na hatua Zangu; msisubiri bila kufanya lolote kwa sababu hii itachelewesha mambo). Ninapowahitaji kutenda katika mwili kama wachungaji wa kanisa, ninyi mtatoka nje ya mwili, muache mawazo yenu, na kunitegemeana kabisa ili kuishi. Muwe na imani katika nguvu Zangu, muwe na imani katika hekima Yangu. Kila kitu kitafanywa na Mimi binafsi. Mnahitaji tu kusubiri kufurahia. Baraka zote zitawajia, na ninyi mtakuwa na ruzuku isiyoisha. Siku hiyo itakapokuja, mtaelewa kanuni ya jinsi Ninavyofanya hivi, mtajua matendo Yangu ya ajabu na kuelewa jinsi Ninavyoleta wana Wangu wazaliwa wa kwanza katika Sayuni. Hili sio gumu kama mnavyofikiria lakini pia si rahisi kama mnavyofikiria.

Najua Ninaposema hili hamwezi hata kwa kiwango cha chini kuelewa madhumuni Yangu katika hilo na huchanganyikiwa zaidi. Mtayachanganya na yale Niliyosema hapo awali ili msiweze kuelewa chochote, itaonekana kama kwamba hakuna njia nyingine. Hata hivyo, msijali, Nitawaambia kila kitu. Kila kitu Ninachosema kina maana. Nimesema kuwa Ninaweza kufanya

vitu vilivyopo virudi kuwa bure na Ninaweza kufanya vitu viwe vingi kutoka kwa utupu. Katika mawazo ya binadamu, kuingia katika mwili kutoka kwa mwili, mtu lazima afufuliwe kutoka kwa wafu. Katika siku za nyuma, Nilitumia njia hii na Nikadhihirisha muujiza Wangu mkuu zaidi, lakini leo si kama zamani. Nitawachukua moja kwa moja kutoka kwa mwili hadi ndani ya mwili. Je, hii sio hata ishara kubwa zaidi na muujiza? Je, huu sio udhihirisho mkubwa zaidi wa kudura Yangu? Nina mpango Wangu, Nina nia Zangu. Nani asiye katika mikono Yangu? Ninafanya kazi na Ninajua. Njia Zangu za kufanya kazi leo ni, hata hivyo, tofauti na zilizopita. Ninabadilisha mbinu Zangu za kufanya kazi kulingana na mabadiliko ya enzi. Wakati Nilipigwa misumari msalabani, hiyo ilikuwa ni Enzi ya Neema, lakini sasa ni enzi ya mwisho. Kasi ya kazi Yangu inaongezeka, sio kasi sawa na ilivyokuwa hapo zamani, sembuse kuwa polepole kuliko siku za nyuma lakini, badala yake, ni haraka zaidi kuliko zamani. Hakuna njia ya kuielezea, hakuna haja ya michakato mingi migumu. Mimi Niko huru kufanya chochote; si kweli kwamba inachukua tu neno moja la mamlaka kutoka Kwangu kuamua jinsi mapenzi Yangu yatakamilishwa na jinsi Nitawakamilisha? Kila kitu Ninachosema hakika kitafanyika. Katika siku za nyuma, mara nyingi Nilisema kuwa nitateseka, na Sikuwaruhusu watu wataje mateso Niliyoyastahimili awali; kutaja hili kulikuwa kunikufuru. Hii ni kwa sababu Mimi ni Mungu Mwenyewe na Kwangu hakuna ugumu; unapotaja mateso haya unawafanya watu walie. Nimesema kuwa katika siku zijazo hakutakuwa na kutanafusi na hakutakuwa na machozi. Inapaswa kuelezwa kutoka kwa mtazamo huu, na kisha maana ya maneno Yangu yanaweza kueleweka. Maana ya “wanadamu hawawezi kustahimili mateso haya” ni kwamba Ninaweza kuondoka kutoka kwa dhana zote za binadamu na fikira, kuachana na hisia za mwili, kuacha dalili yoyote ya kuwa wa kupenda anasa za ulimwengu na kuondoka katika mwili, na bado Ninaweza kusimama wakati kila mtu ananikana Mimi. Hii inatosha kuthibitisha kuwa Mimi ni Mungu Mwenyewe wa pekee. Nimesema, “Kila mwana mzaliwa wa kwanza lazima aingie katika ulimwengu wa kiroho kutoka kwa mwili; hii ndiyo njia ambayo wanapaswa kuchukua ili kutawala pamoja nami kama wafalme.” Maana ya sentensi hii ni kwamba unapokumbana na kitu ambacho mnacho, zamani, mlifikiri, mtaondoka rasmi katika nyama na kuingia katika mwili ili muanze kuwahukumu rasmi wale wana wa wafalme na wafalme hao. Wao watahukumiwa kulingana na mambo yanayotokea wakati huu. Hata hivyo, sio ngumu kama mnavyofikiria, itafanyika papo hapo. Hamtahitaji kufufuka kutoka kwa wafu na hamtahitaji hata kuteseka (kwa sababu mateso na shida zenu duniani tayari zimekamilika na Nimekwisha kusema kuwa Sitashughulika tena na wanangu wazaliwa wa kwanza baada ya hapo). Wazaliwa wa kwanza watafurahia baraka zao, kama ilivyoongelewa, kwa kweli kwamba mtaingia katika ulimwengu wa kiroho bila kujua. Kwa nini Nasema kuwa hii ni rehema Yangu na neema? Ikiwa mtu angeweza tu kuingia katika ulimwengu wa kiroho baada ya kufufuka kutoka kwa wafu, hii ingekuwa mbali na kuwa ya huruma na neema. Kwa hivyo haya ndiyo maonyesho ya dhahiri

zaidi ya rehema Yangu na neema na, zaidi ya hayo, yanafichua uamuzi Wangu kabla na uteuzi Wangu wa watu. Inatosha kuonyesha jinsi amri Yangu ya utawala ilivyo kali. Nitakuwa mwenye huruma kwa yeyote Nitakayetaka na kuwa mwenye huruma kwa yeyote Nitakayetaka. Hakuna mtu atakayepinga au kupigana. Nitaamua yote haya.

Watu hawawezi kuelewa hilo na wanajiwekea shinikizo mpaka wasiweze kupumua na bado wanajifunga. Mawazo ya watu ni finyu sana, kwa hiyo ni lazima watupilie mbali mawazo na dhana za binadamu. Kwa hivyo, ni lazima Nitoke katika mwili na kuingia katika ulimwengu wa kiroho kuchukua udhibiti wa kila kitu, kusimamia kila kitu. Hii ndiyo njia pekee ya kutawala watu wote na mataifa yote na kutimiza mapenzi Yangu. Sio mbali sana. Hamna imani katika kudura Yangu, hamjui mwanadamu Niliye. Mnafikiri kwamba Mimi ni mtu tu, hamwezi kuona uungu Wangu hata kidogo. Mambo yatakuwa kamili wakati wowote Ninapotaka yawe kamili. Kinachohitajika tu ni neno kutoka katika kinywa Changu. Ninyi mmetilia maanani tu kipengele cha ubinadamu Wangu katika kile ambacho Nimesema hivi karibuni na kila Ninachofanya, lakini hamjatilia maanani kipengele cha uungu Wangu. Hiyo ni kusema kwamba mnadhani kwamba Mimi pia nina mawazo na dhana. Lakini Nimesema kuwa fikira Zangu, mawazo na akili, kila Ninachofanya, kila kitu Ninachotenda na kila kitu Ninachosema ni udhihirisho kamili wa Mungu Mwenyewe. Je, mmesahau yote haya? Ninyi nyote ni watu waliochanganyikiwa! Hamwelewi maana ya maneno Yangu. Nimewaruhusu kuona kipengele cha ubinadamu Wangu wa kawaida kutoka kwa kile Nilichosema (Nimewawezesha kuona ubinadamu Wangu wa kawaida katika maisha Yangu ya kila siku, kwa kweli, kwa sababu ninyi bado hamwelewi kipengele cha ubinadamu Wangu wa kawaida kutokana na kile Nilichosema wakati huu), ilhali hamwelewi ubinadamu Wangu wa kawaida, na mnajaribu kushikilia tu kitu ambacho kinaweza kutumiwa dhidi Yangu na mnakuwa bila nidhamu mbele Yangu. Ninyi ni vipofu! Ninyi ni wapumbavu! Hamnijui Mimi! Nimenena bure kwa muda mrefu, ninyi hamnijui Mimi kabisa, hamuchukulii ubinadamu Wangu wa kawaida kama sehemu ya Mungu Mwenyewe mkamilifu kabisa! Ninawezaje kukosa kuwa na hasira? Ninawezaje kuwa mwenye huruma tena? Ninaweza tu kuwajibu watoto hawa wa kutotii na hasira Yangu. Wenye kiburi sana, wasionijua sana! Mnafikiria kwa mwanadamu Niliye amefanya makosa! Naweza kufanya makosa? Ningechagua bila mpango kuuchukua mwili wowote? Ubinadamu Wangu na uungu Wangu ni sehemu mbili zisizoweza kutenganishwa ambazo zinajumuisha Mungu Mwenyewe mkamilifu. Sasa mnapaswa kuelewa vizuri kuhusu hili! Maneno Yangu tayari yamefikia kilele chayo, na maneno Yangu hayawezi tena kuelezwa kwa urefu zaidi!

Sura ya 99

Kwa sababu mwendo wa kazi Yangu unaongeza kasi, hakuna anayeweza kuenda mwendo

sawa na nyayo Zangu, na hakuna anayeweza kupenya akili Yangu, bado hii ndiyo njia tu ya kwenda mbele. Hii ni “mfu” (ikiashiria kukosa uwezo wa kuelewa kile Ninachomaanisha kutoka kwa maneno Yangu; hii ni njia mbadala ya kueleza “mfu”, na haimaanishi “kuachwa na Roho Wangu”) katika msemo “kufufuka kutoka wafu”, ambako kumeshazungumziwa. Wakati nyinyi na Mimi tumebadilika kutoka kwa awamu hii hadi kwenye mwili, basi maana halisi ya “kufufuliwa kutoka wafu” itatimizwa (yaani, hii ni maana halisi ya ufufuko kutoka kwa wafu). Sasa, hii ni hali ambamo nyote mko: Hamwezi kufahamu mapenzi Yangu na hamwezi kupata nyayo Zangu. Zaidi ya hayo, hamwezi kuwa kimya katika mioyo yenu, hivyo mnahisi msio na utulivu katika akili. Hali ya aina hii hasa ni “mateso” Niliotaja, na ndani ya haya mateso, ambayo watu hawawezi kustahimili, mnafikiri kuhusu siku zenu za baadaye wenyewe, na kwa upande mwingine mnakubali kuchomwa na Mimi, hukumu Yangu, yakija ghafla kwenu kutoka kila upande. Zaidi ya hayo, kwa sauti na jinsi ambavyo Mimi huongea, hamwezi kufahamu kanuni zozote, na kwa siku moja ya tamko kuna aina kadhaa ya sauti, ili mteseke sana. Hizi ndizo hatua katika kazi Yangu. Hii ndiyo hekima Yangu. Baadaye mtapitia, mateso makubwa zaidi kuhusu hili, yote ambayo ni ili kufichua watu wote wanafiki—hili linapaswa kuwa dhahiri sasa! Hii ndiyo njia Nifanyayo kazi. Kuwa na motisha ya aina hii ya mateso, na baada ya kuupitia uchungu huu ambao ni sawa na kifo, mtaingia katika eneo jingine. Mtaingia katika mwili na kutawala mataifa yote na watu wote nami.

Kwa nini hivi karibuni Nimekuwa nikiongea kwa sauti kali zaidi? Kwa nini sauti Yangu imebadilika mara kwa mara sana na kwa nini njia Yangu ya kufanya kazi pia imebadilika mara kwa mara sana? Hekima Yangu imekuwa katika vitu hivi. Maneno Yangu yanasemwa kwa ajili ya kila mtu ambaye amekubali jina hili (iwapo wanaamini maneno Yangu yanaweza kutimizwa au la), hivyo maneno Yangu yanapaswa kusikizwa na kuonwa na kila mtu, na sharti yasikandamizwe kwa sababu Nina njia Yangu ya kufanya kazi na Nina hekima Yangu. Natumia maneno Yangu kuhukumu watu, kufichua watu, na kuweka wazi asili ya binadamu. Kwa hivyo, Nateua wale ambao Nachagua, na kwa hivyo Naondoa wale ambao Sijajaalia au kuchagua. Haya yote ni hekima Yangu na ajabu ya kazi Yangu. Hii ni mbinu Yangu hasa katika awamu hii ya kazi Yangu. Kati ya watu, kuna yeyote anayeweza kufahamu mapenzi Yangu? Kati ya watu, kuna yeyote anayeweza kufikiria mzigo Wangu? Anayefanya kazi ni Mimi, Mungu Mwenyewe. Kutakuwa na siku, mtakapoelewa kabisa umuhimu wa maneno haya Yangu, na mtakuwa dhahiri kabisa kuhusu kwa nini Nataka kuongea maneno haya. Hekima Yangu haina mwisho, haina kikomo, na haiwezi kupimika, na haiwezi kupenyeka kabisa na wanadamu. Wanaweza kuona tu sehemu yake kutoka kwa vitu Mimi hufanya, lakini kile wanachoona bado kina dosari na bado si kamili. Wakati ambapo mmebadilika kabisa kutoka kwa awamu hii hadi kwa awamu inayofuata, basi mtakuwa na uwezo wa kuiona dhahiri. Kumbukeni! Sasa ndiyo enzi ya thamani zaidi—ni

awamu ya mwisho ambayo mtakuwa katika mwili. Maisha yenu sasa hivi ni mwisho wa maisha yenu ya kimwili. Mnapoingia dunia ya kiroho kutoka kwa mwili, wakati huo maumivu yote yatawaacha. Mtafurahia na kushangilia sana, na mtaruka kwa shangwe bila kuacha. Lakini lazima muwe dhahiri kwamba maneno haya Ninayoongea ni ya wazaliwa wa kwanza tu, kwa sababu wazaliwa wa kwanza tu ndio wanaostahili baraka hii. Kuingia katika dunia ya kiroho ndiyo baraka kuu zaidi, baraka ya juu zaidi, na raha ya thamani zaidi. Sasa kile mnachopata kula na kile mnachopata kuvaa si chochote zaidi ya raha za mwili, na ni neema, ambayo Sijali kamwe. Lengo la kazi Yangu liko katika awamu inayofuata (kuingia katika dunia ya kiroho na kukabili ulimwengu dunia).

Nimesema kwamba joka kubwa jekundu tayari limerushwa chini na Mimi na kupondwa. Mnawezaje kukosa kuyaamini maneno Yangu? Kwa nini bado mnatamani kuvumilia mateso na dhiki kwa ajili Yangu? Je, hii si gharama ya isiyojaa nyinyi kuilipa? Nimewakumbusha mara nyingi kwamba mnahitaji tu kuona raha, wakati Nafanya kazi kibinafsi: Kwa nini mna hamu sana ya kuchukua hatua? Kwa kweli hamjui jinsi ya kuona raha! Nimetayarisha kabisa kila kitu kwa ajili yenu: Kwa nini hakuna kati yenu ambaye amekuja Kwangu kukichukua? Bado hamna uhakika kuhusu kile Nimesema! Hamnielewi! Mnadhani kwamba Ninaongea masihara matupu na nyinyi ni wapumbavu kweli! (Matayarisho kamili Ninayoongea kuhusu yanamaanisha kwamba mnapaswa kuniheshimu zaidi na kuomba zaidi mbele Yangu, wakati Nitafanya kazi kibinafsi kulaani kila mmoja ambaye hunipinga, na kuadhibu kila mmoja anayewatesa.) Nyinyi hamjui chochote kuhusu maneno Yangu! Nafichua mafumbo Yangu yote kwenu, na wangapi kati yenu wanayaelewa kweli? Wangapi kati yenu wanayaelewa kwa kina? Kiti Changu cha enzi ni nini? Fimbo Yangu ya chuma ni nini? Nani kati yenu anajua? Kiti Changu cha enzi kinapotajwa, watu wengi zaidi hufikiri hapo ndipo Ninapoketi, au kwamba kinarejelea makazi Yangu, kwa Yule mtu Niliye. Huu wote ni ulewa usio sahihi—ni fujo yenye mkanganyo kabisa! Hakuna kati ya uelewa huu ambao ni sahihi, sivyo? Hii ndiyo njia nyinyi nyote mnalielewa na kulifahamu—huku ni kupotoka kwa kukithiri kwa ufahamu! Mamlaka ni nini? Ni nini uhusiano kati ya mamlaka na kiti cha enzi? Kiti cha enzi ni mamlaka Yangu. Wazaliwa Wangu wa kwanza wanapotukuza kiti Changu cha enzi, huo ndio wakati ambao wazaliwa Wangu wa kwanza watapokea mamlaka kutoka Kwangu. Mimi tu ndiye niliye na mamlaka, hivyo Mimi tu ndiye niliye na kiti cha enzi. Kwa maneno mengine, baada ya wazaliwa Wangu wa kwanza kuteseka kwa njia sawa na Nilivyoteseka, watakubali kile Nilicho na kile Ninacho, na watapokea kila kitu kutoka kwangu, na huu ndio mchakato ambao kwao watafikia hadhi ya mzaliwa wa kwanza. Utakuwa wakati wazaliwa Wangu wa kwanza watakapotukuza kiti Changu cha enzi, na utakuwa wakati ambapo watakubali mamlaka kutoka kwangu. Sasa mnapaswa kuelewa hili! Kila kitu Ninachosema ni dhahiri na kisichokuwa na utata kabisa ili kila mtu aelewa. Wekeni kando dhana

zenu wenyewe, na ngojeni kukubali mafumbo ambayo Nafichua kwenu! Hivyo ni nini fimbo ya chuma? Katika awamu iliyopita ilimaanisha maneno Yangu makali, lakini sasa ni tofauti na zamani: Sasa fimbo ya chuma hurejelea matendo Yangu, ambayo ni misiba mikuu inayobeba mamlaka. Kwa hivyo, kwa kutajwa fimbo ya chuma, iko pamoja na mamlaka, Maana ya awali ya fimbo ya chuma inarejelea misiba mikuu—ni sehemu ya mamlaka. Kila mtu lazima aone hili dhahiri na hivyo tu ndipo anaweza kufahamu mapenzi Yangu na kupokea ufunuo kutoka kwa Maneno Yangu. Yeyote ambaye ana kazi ya Roho Mtakatifu hushikilia fimbo ya chuma katika mkono wake, na ni yeye ambaye ana mamlaka na ana haki ya kutekeleza misiba yoyote mikuu. Hiki ni kishazi kimoja cha amri Yangu ya utawala.

Kila kitu kiko wazi kwenu (kurejelea sehemu ambayo imesisitizwa dhahiri), na kila kitu kinafichwa kutoka kwenu (kurejelea sehemu ya siri ya maneno Yangu) Nazungumza hekima: Nawaruhusu muelewe tu maana halisi ya baadhi ya maneno Yangu, Nikiwaruhusu kufahamu maana ya mengine (lakini watu wengi zaidi hawana uwezo wa kuelewa), kwa sababu huu ndio mpangilio wa kazi Yangu. Ninaweza tu kuwaambia maana ya kweli ya maneno Yangu wakati mtafika kimo fulani. Hii ni hekima Yangu na haya ni matendo Yangu ya ajabu (ili kuwakamilisha na ili kumshinda Shetani kabisa na kuaibisha maibilisi). Si hadi muingie katika eneo jingine ndipo mtakuwa na uwezo wa kuelewa kabisa. Lazima Nifanye kwa njia hii kwa sababu katika dhana za binadamu kuna vitu vingi watu hawawezi kuelewa kabisa, na hata Nikiongea dhahiri bado hamtaelewa. Akili za watu ni, hata hivyo, finyu, na kuna vitu vingi ambavyo Ninaweza tu kuwasilisha kwenu baada ya nyinyi kuingia katika dunia ya kiroho; vinginevyo, mwili wa binadamu ni hafifu na hili linaweza tu kuvuruga usimamizi Wangu. Hii ndiyo maana ya kweli ya “mpangilio wa kazi Yangu” Ninayoongea kuhusu. Katika dhana zenu mnanielewa kwa kiasi gani? Uelewa wenu hauna dosari? Je, ni maarifa mnayo katika roho? Kwa hivyo, lazima Niwaruhusu mbadilike kuingia katika eneo jingine ili mkamilishe kazi Yangu na kufanya mapenzi Yangu. Hivyo ni nini hasa eneo hili jingine? Je, kwa kweli ni, aina ya mtazamo wa uvukaji mipaka, kama wafikiriavyo watu? Je, kwa kweli ni kitu kama hewa ambacho hakiwezi kuonekana ama kuguswa, ilhali kipo? Kama Nilivyosema, hali ya kuwa katika mwili ni ile ya kuwa na nyama na mfupa—iliyo na muundo na umbo. Hili ni kweli kabisa na la kuaminika, na kila mtu lazima aliamini. Huu ndio uhalisi katika hali ya kimwili. Zaidi ya hayo, katika mwili hakuna mambo ambayo watu huchukia. Lakini hali hii ni nini hasa? Watu wanapopita kutoka kwa nyama hadi kwa mwili, kundi kikubwa lazima kijitokeze. Hiyo ni kusema, watatoroka kutoka kwa makazi yao ya kimwili, na inaweza kusemwa kwamba kila atafuata aina yake mwenyewe: Nyama hukusanyika kwa nyama na mwili hukusanyika kwa mwili. Sasa wale wanaotoroka kutoka kwa makazi yao, wazazi wao, wake, waume, wana, na binti, huanza kuingia katika dunia ya kiroho. Mwishoni, ni njia hii: Hali katika dunia ya kiroho

ni kwamba wazaliwa wa kwanza wanakusanyika pamoja, wakiimba na kucheza, kusifu na kushangilia jina Langu takatifu. Na hili ni tukio ambalo ni zuri na jipya daima. Wote ni wana Wangu wapendwa, daima wakinisifu bila kuacha, daima wakitukuza jina Langu takatifu. Hii ndiyo hali baada ya kuingia katika dunia ya kiroho, hii pia ni kazi baada ya kuingia katika dunia ya kiroho, na hii pia ndiyo hali ambayo Nimeongea kuhusu, ya kuchunga kanisa katika dunia ya kiroho. Zaidi ya hayo, ni kwamba nafsi Yangu huonekana katika kila taifa la ulimwengu na kati ya mataifa yote na watu wote, ikiwa na mamlaka Yangu, ghadhabu Yangu, na hukumu Yangu, na hata zaidi, ikiwa na fimbo Yangu ya chuma kutawala mataifa yote na watu wote. Hili, kati ya watu wote na ulimwengu mzima, hutoa ushahidi Kwangu unaotetemesha mbingu na ardhi, ukisababisha watu wote na vitu vyote juu ya milima, ndani ya mito, ndani ya maziwa, na katika miisho ya dunia kunisifu na kunitukuza, na kunijua, Mungu mmoja Mwenyewe, Muumba wa vitu vyote, Anayeongoza kila kitu, husimamia kila kitu, huhukumu kila kitu, hufanikisha kila kitu, huadhibu kila kitu, na huangamiza kila kitu. Huku, basi, ni kuonekana kwa nafsi Yangu.

Sura ya 100

Ninawachukia wale wote ambao hawajajaaliwa na kuchaguliwa na Mimi. Kwa hiyo ni lazima Niwafukuze watu hawa kutoka katika nyumba Yangu mmoja baada ya mwingine, hivyo hekalu Langu litakuwa takatifu na bila doa, nyumba Yangu itakuwa mpya daima na haitakuwa nzee kamwe, jina Langu takatifu litaenezwa milele na watu Wangu watakatifu watakuwa wapendwa Wangu. Aina hii ya mandhari, aina hii ya nyumba, aina hii ya ufalme ni lengo Langu, makao Yangu nayo ni msingi wa uumbaji Wangu wa vitu vyote. Hakuna mtu anayeweza kuyayumbisha au kuyabadilisha. Mimi mwenyewe na wana Wangu wapendwa tutaishi pamoja ndani yake na hakuna mtu atakayeruhusiwa kuyakanyaga, hakuna chochote kitakachoruhusiwa kuishi humo na hata zaidi hakuna kitu chochote kibaya kitakachoruhusiwa kutokea kamwe. Yote itakuwa sifa na kushangilia tu, yote yatakuwa mandhari ambayo mwanadamu hawezi kudhania. Natamani tu kwamba mtatoa nguvu zenu zote Kwangu kwa mioyo yenu yote na akili zenu zote na kadri ya uwezo wenu. Kama leo au kesho, kama wewe ni mtu ambaye anatoa huduma kwa ajili Yangu au mtu anayepata baraka, nyote mnapaswa kutumia sehemu ya nguvu zote kwa ajili ya ufalme Wangu. Huu ni wajibu ambao watu wote walioumbwa wanapaswa kutekeleza, nao unapaswa kufanywa na kutekelezwa kwa njia hii. Nitavihamasisha vitu vyote vitoe huduma kwa uzuri wa ufalme Wangu ili ufanywe mpya daima, na nyumba Yangu ifanywe kuwa yenye mpangilio mzuri na yenye umoja. Hakuna mtu anayeruhusiwa kunipinga Mimi, na anapaswa kupitia hukumu na kulaaniwa. Sasa laana Zangu zinaanza kuyashambulia mataifa yote na watu wote na laana Zangu ni kali hata zaidi kuliko hukumu. Sasa ni wakati wa kuanza kuwahukumu watu wote, kwa hivyo inasemwa kuwa ni laana. Hii ni kwa sababu sasa ni enzi ya mwisho na si wakati wa uumbaji. Kwa kuwa enzi zimebadilika, kasi ya kazi Yangu sasa ni tofauti sana.

Kutokana na mahitaji ya kazi Yangu, watu Ninaowahitaji pia ni tofauti; wale ambao wanapaswa kutelekezwa watatelekezwa; wale ambao wanapaswa kutengwa watatengwa; wale ambao wanapaswa kuuawa watauawa na wale ambao wanapaswa kuachwa lazima waachwe. Huu ni mwenendo usioepukika ambao hautegemei dhamira ya mwanadamu na hakuna mtu anayeweza kuubadilisha. Lazima ufanyike kulingana na mapenzi Yangu! Nawaacha wale ambao Nitawaacha na kuwaondoa wale ambao Nitawaondoa; hakuna atakayetenda kiholela. Nawaacha wale ambao Nataka kuwaacha na Ninawapenda wale ambao Nataka kuwapenda; lazima jambo hili lifanyike kulingana na mapenzi Yangu! Sitendi kwa kusukumwa na hisia; Pamoja nami kuna haki, hukumu na hasira tu—hakuna hisia hata kidogo. Hakuna dalili hata kidogo ya ubinadamu ndani Yangu, kwa maana mimi ni Mungu Mwenyewe, nafsi ya Mungu. Kwa sababu watu wote wanaona kipengele Changu ambacho ni ubinadamu Wangu na hawajaona kipengele ambacho ni uungu Wangu. Wao kweli hawatambui nao wamevurugika sana!

Lazima mzingatie Ninachowaambia mioyoni mwenu, lazima muuelewe moyo Wangu kupitia kwa maneno Yangu na muufikirie kwa makini mzigo wangu, na hivyo mtakuja kuujuu uweza Wangu na kuiona nafsi Yangu. Kwa kuwa maneno Yangu ni maneno ya hekima na hakuna mtu anayeweza kufahamu kanuni au sheria za maneno Yangu. Watu wanadhani kwamba natenda ulaghai na udanganyifu nao hawanijui kupitia kwa maneno Yangu, lakini badala yake wananikufuru. Wao ni wazembe na wajinga sana! Na hawana ufahamu wowote. Kila sentensi Ninayotamka huwa na mamlaka na hukumu na hakuna mtu anayeweza kuzibadilisha. Mara tu maneno Yangu yanapotoka, mambo yatafanyika kwa mujibu wa maneno Yangu, na hii ndiyo tabia Yangu. Maneno Yangu ni mamlaka na yeyote anayeyarekebisha hukosea kuadibu Kwangu na ni lazima Nimwangamize. Hali ikiwa mbaya hayo husababisha uharibifu katika maisha yao wenyewe nao huenda kuzimu, au huenda jahanamu. Hii ndiyo njia ya pekee ambayo kwayo Ninawashughulikia wanadamu na mwanadamu hawezi kuibadilisha—hii ni amri Yangu ya utawala. Kumbuka hili! Hakuna mtu anayeruhusiwa kuikosea amri Yangu; lazima hili lifanyike kulingana na mapenzi Yangu! Zamani Nilikuwa mpole sana kwenu nanyi mlikabiliwa na maneno Yangu tu. Maneno Niliyonena kuhusu kuwaangamiza watu hayajatokea bado. Lakini kuanzia leo, majanga yote (haya yanayohusiana na amri Zangu za utawala) yatatokea moja baada ya lingine ili yawaadhibu wale wote wasiotii mapenzi Yangu. Lazima kuwe na ujio wa ukweli, vinginevyo watu hawataweza kuona ghadhabu Yangu lakini watapotoshwa tena na tena. Hii ni hatua ya mpango Wangu wa usimamizi nayo ni njia ambayo kwayo Mimi kushughulikia hatua inayofuata ya kazi Yangu. Nawaambieni hivi mapema ili muweze kuepuka kufanya makosa na kupitia mateso milele. Hiyo ni kusema, kuanzia leo Nitawafanya watu wote ila wazaliwa Wangu wa kwanza kuchukua nafasi zao halisi kwa mujibu wa mapenzi Yangu, nami Nitawaadibu mmoja baada ya mwingine. Sitamsamehe hata mmoja wao. Hebu thubutu tu kuwa wapotovu

tena! Hebu thubutu tu kuwa mwasi tena! Nimesema mbeleni kuwa Mimi ni mwenye haki kwa wote bila hisia yoyote, na huu ni mfano kwamba tabia Yangu haipaswi kukosewa. Hii ni nafsi Yangu. Hakuna mtu anayeweza kubadilisha jambo hili. Watu wote husikia maneno Yangu na watu wote huuona uso Wangu mtukufu. Watu wote wanapaswa kunitii kabisa na kwa ukamilifu—hii ni amri Yangu ya utawala. Watu wote katika ulimwengu mzima na katika miisho ya dunia wanapaswa kunisifu na kunitukuza, kwa maana Mimi ni Mungu Mwenyewe wa pekee, kwa maana Mimi ni nafsi ya Mungu. Hakuna mtu anayeweza kubadili maneno na matamshi Yangu, usemi na mwenendo Wangu, kwa kuwa haya ni mambo Yangu peke Yangu, na kile ambacho Nimemiliki tangu milele na kile ambacho kitakuwepo milele.

Watu wana nia ya kunijaribu, nao wanataka kutafuta kitu ambacho wanaweza kutumia dhidi Yangu ndani ya maneno Yangu, ili wanikashifu. Je, Ninapaswa kukashifiwa nawe? Je! Ninapaswa kuhukumiwa kiholela? Je, shughuli Zangu zapaswa kujadiliwa kiholela? Kweli ninyi ni kikundi cha watu wasiojua kinachowafaa! Hamnijui kabisa! Mlima Sayuni ni nini? Makao Yangu ni nini? Nchi nzuri ya Kanaani ni nini? Msingi wa uumbaji ni nini? Kwa nini Nimekuwa Nikiendelea kutaja maneno haya kwa siku chache zilizopita? Mlima Sayuni, makao Yangu, nchi nzuri ya Kanaani, msingi wa uumbaji, vyote vinasemwa kuhusu nafsi Yangu (kuhusu mwili). Watu wote wanadhani kuwa hayo ni maeneo ambayo yapo kihalisi. Nafsi Yangu ni Mlima Sayuni nayo ni makao Yangu. Yeyote anayeingia katika ulimwengu wa kiroho ataupanda Mlima Sayuni, naye ataingia katika makao Yangu. Niliumba vitu vyote ndani ya nafsi Yangu, yaani, vitu vyote viliumbwa ndani ya mwili, kwa hiyo ni msingi. Kwa nini Nasema kwamba mtarudi katika mwili pamoja na Mimi? Humo mna maana ya asili. Kama vile tu jina “Mungu,” majina haya hayana maana kwayo yenyewe, bali ni majina tofauti Ninayozipa sehemu tofauti. Kwa hiyo usizingatie sana maana yao halisi, lakini sisitiza tu katika kusikia maneno Yangu. Lazima uyaelewe kwa njia hii na kisha utaweza kufahamu mapenzi Yangu. Kwa nini Nawakumbusha tena na tena kwamba kuna hekima katika maneno Yangu? Ni wangapi kati yenu wamejaribu kufahamu maana ya jambo hili? Ninyi nyote mnayachunguza bila kufikiri na mnakosa mantiki!

Bado sasa hamwelewi mambo mengi ambayo Nimesema katika siku zilizopita. Mnabaki katika hali ya shaka na hamuwezi kuukidhi moyo Wangu. Wakati wowote mnaweza kuwa na uhakika kuhusu kila sentensi Ninayonena, huo utakuwa wakati ambao maisha yenu yanakua. Kwangu, siku moja ni kama miaka elfu na miaka elfu kama siku moja; Je! Mnaonaje kuhusu wakati Ninaozungumzia? Je, mnauelezeaje? Mnauelewa vibaya! Na zaidi ya hayo watu wengi bado wanashindana kuhusu jambo hili nami, wakitamani kupata kitu cha kutumia dhidi Yangu—hamjui ni nini kinachowafaa! Kuwa mwangalifu, kwani vinginevyo Nitakuangamiza! Siku itakapowadia ambapo kila kitu kinafafanuliwa mtaelewa kabisa. Bado Siwaambii sasa (sasa ni wakati wa kuwafunua watu na sharti kila mtu awe mwangalifu na mwenye busara ili aweze

kuyakidhi mapenzi Yangu). Nitawafichua watu wote kupitia maneno Yangu na maumbo yao ya asili yatafichuliwa ili kuonyesha kama ni kweli au la. Ikiwa mtu ni kahaba au malaya, lazima Nimfichue. Nimesema awali kwamba Ninafanya mambo bila kujitahidi kufanya lolote na kwamba Ninatumia maneno Yangu pekee kuwafichua watu. Mimi siogopi hila yoyote; baada ya kunena maneno Yangu, bila shaka lazima ufichue umbo lako la asili, na haijalishi jinsi unavyojificha kwa hakika Nitatambua hilo. Hii ni kanuni ya matendo Yangu—kutumia matamshi tu na sio kutumia nguvu yoyote ile. Watu huwa na woga na wasiwasi kuhusu kama maneno Yangu yatatimizwa au la, wanakuwa na wasiwasi kwa ajili Yangu na wanahangaika kwa ajili Yangu, lakini jitihada hizi hazihitajiki kwa kweli nao ni matokeo ambayo hayafai. Una wasiwasi juu Yangu lakini je, maisha yako mwenyewe yamekomaa? Je kuhusu kudura yako mwenyewe? Jiulize mara nyingi na usiwe hobelahobela. Watu wote wanapaswa kuizingatia kazi Yangu na—kupitia matendo Yangu na maneno Yangu—waione nafsi Yangu, wawe na ujuzi zaidi kunihusu Mimi, wajue uweza Wangu, wajue hekima Yangu na wajue njia na mbinu ambazo kwazo Niliumba vitu vyote, na hivyo kunipa sifa ya kudumu. Nitawafanya watu wote waone mikono ya amri Zangu za utawala ziko juu ya nani, nani ambaye Ninafanyia, ni nini Ninachotaka kufanya na ni nini Ninachotaka kukamilisha. Hili ni jambo ambalo kila mtu anapaswa kutimiza, kwa maana hii ni amri Yangu ya utawala. Nitatimiza kile Ninachosema. Hakuna mtu anayepaswa kuyachambua maneno Yangu kwa kawaida, wote wanapaswa kuona kanuni za matendo Yangu kupitia kwa maneno Yangu, na kutoka kwa maneno Yangu wajue hasira Yangu ni nini, laana Yangu ni nini na hukumu Yangu ni nini. Mambo haya yote yanategemea maneno Yangu na ni mambo ambayo yanapaswa kuonekana na kila mtu ndani ya kila moja ya maneno Yangu.

Sura ya 101

Sitakuwa mwenye huruma kwa yeyote anayeingilia usimamizi Wangu ama anayejaribu kuiharibu mipango Yangu. Kila mtu anapaswa kuelewa kile Ninachomaanisha kutoka kwa maneno Ninayosema na lazima aelewe vizuri kile Ninachozungumzia. Kwa kuzingatia hali iliyopo, kila mtu anapaswa kujichunguza: Ni wajibu gani unaotekeleza? Unaishi kwa ajili Yangu, au unamtumikia Shetani? Je, kila moja ya matendo yako hutoka Kwangu, au hutoka kwa Shetani? Haya yote yapaswa kuwa dhahiri ili kuepuka kukosea amri Zangu za utawala na hivyo kupata ghadhabu Yangu. Tukiangalia nyuma, daima watu hawajakuwa waaminifu na wamenikaidi, wamenikosea heshima, na zaidi ya hayo, wamenisaliti. Kwa sababu hizi watu hawa wanapitia hukumu Yangu leo. Japo Ninaonekana kama mwanadamu tu, wale wote ambao Sijawakubali (unapaswa kuelewa maana Yangu kutokana na hili: Sikuhusu jinsi unavyoonekana kuwa mrembo ama jinsi unavyopendeza, bali kama Nimekujaalia na kukuchagua) watakuwa walengwa wa kuangamizwa na Mimi. Huu ni ukweli kabisa. Kwa kuwa Ninaweza kuonekana

kama mwanadamu, lakini unahitaji kutozingatia ubinadamu Wangu ili uufahamu uungu Wangu. Nimesema mara nyingi, “Ubinadamu wa kawaida na uungu kamili ni sehemu mbili zisizotengana za Mungu Mwenyewe mkamilifu.” Hata hivyo, bado hamnielewi, na bado mnamzingatia tu Mungu wenu asiye dhahiri. Ninyi ni watu msioelewa mambo ya kiroho. Lakini watu wa aina hiyo bado wanataka kuwa wazaliwa Wangu wa kwanza. Ni fedheha iliyoje! Hawaoni hadhi yao wenyewe ilivyo kwa kweli! Hata hawastahili kuwa watu Wangu, wangepewe kuwa wazaliwa Wangu wa kwanza ambao wangukuwa wafalme pamoja na Mimi? Watu wa aina hii hawajijui, ni wa kabila la Shetani; hawastahili kuwa nguzo katika kaya Yangu, na hawafai kunitumikia hata kidogo. Kwa hivyo Nitawaondoa mmoja baada ya mwingine, na Nitafichua tabia zao za kweli.

Kazi Yangu inaendelea hatua kwa nyingine bila kuzuiliwa na bila pingamizi lolote kwa sababu Nimepata ushindi na kwa sababu Nimetawala kama Mfalme ulimwenguni kote. (Kile Ninachozungumzia ni kuwa baada ya kumshinda ibilisi Shetani Nimetwaa upya uongozi Wangu.) Ninapowapata wazaliwa Wangu wa kwanza wote, basi bendera ya ushindi itapepea juu ya Mlima Sayuni. Hiyo ni kusema, wazaliwa Wangu wa kwanza ni bendera Yangu ya ushindi, utukufu Wangu, sababu Yangu ya kujisifia; wao ni ishara kuwa Nimemuaibisha Shetani nao ni mbinu ambayo kwayo Ninafanya kazi. (Kupitia kwa kundi la watu waliopotoshwa na Shetani baada Yangu kuwajaalia, lakini waliorudi upande Wangu upya, Ninaliaibisha joka kuu jekundu na kuwatawala wana wote wa uasi.) Wazaliwa Wangu wa kwanza wako mahali uenyezi Wangu uko, wao ni ufanisi Wangu mkuu, wasiobadilika na wasiopingika. Ni kupitia kwa wazaliwa Wangu wa kwanza ndipo Nitakapoukamilisha mpango Wangu wa usimamizi, Nilimaanisha hivi kitambo Niliposema: “Ni kupitia kwenu ndipo Nitayasababisha mataifa yote na watu wote kurudi mbele ya kiti Changu cha enzi.” Zaidi ya hayo, ndivyo Nilivyomaanisha kwa kusema “mzigo mzito mabegani mwenu.” Hilo ni dhahiri? Mnaelewa? Wazaliwa wa kwanza ni dhihirisho la mpango Wangu wote wa usimamizi. Kwa hiyo, Sijawahi kulitendea kundi hili kwa upole, na kila mara Nimewafundisha nidhamu kwa ukali(adhabu hiyo kali ikiwa ni mateso yanayopitiwa duniani, misiba ya familia, kuachwa na wazazi, waume, wake, na watoto. Kwa jumla, kuachwa na ulimwengu na kutelekezwa na enzi), na hii ndiyo maana una bahati nzuri ya kuja mbele Zangu leo. Hili ndilo jawabu la swali ambalo mmeuliza mara kwa mara kuhusu “Kwa nini watu wengine hawakulikubali jina hili, lakini Mimi Nililikubali?” Sasa Mnajua!

Leo hakuna chochote kilicho sawa na hapo zamani. Mpango Wangu wa usimamizi umechukua mbinu mpya, kazi Yangu ni tofauti hata zaidi na ilivyokuwa hapo zamani na matamshi Yangu sasa ni ya kipekee hata zaidi. Kwa hiyo, Nimesisitiza mara kwa mara kwamba sharti mnitumikie kwa usahihi (hili linasemwa kwa watendaji huduma). Msijitendee kwa njia isiyojaa, lakini endeleeni kufuatilia kwa bidii. Je, haipendezi kupata neema kiasi? Ni bora zaidi

kuliko kuteseka duniani. Nakuambia! Usiponihudumia kwa moyo wote, na badala yake ulalamike kwamba nimekuwa mdhalimu, basi kesho utaelekea kuzimu na jahanamu. Hakuna mtu anayetaka kufa mapema, sivyo? Hata ikiwa ni siku moja zaidi tu, ni siku yenye thamani, sasa utajitolea kabisa kwa mpango Wangu wa usimamizi na baadaye usubiri hukumu Yangu kwako na usubiri kuadibu Kwangu kwa haki kukufike. Usidhani Niyanenayo ni upuuzi; Ninanena kutoka kwa haki Yangu na kutoka kwa tabia Yangu, na zaidi ya hayo Ninatenda kwa uadhama na haki Yangu. Watu wanasema kuwa Mimi ni mdhalimu. Hii ni kwa sababu hawanifahamu. Ni dhihirisho wazi la tabia yao ya uasi. Kwangu hakuna hisia, badala yake kuna haki, uadhama, na ghadhabu tu. Kadri muda unavyoendelea kusonga ndivyo mtakavyoiona tabia Yangu. Wakati huu ni kipindi cha mpito, nanyi mnaweza kuona sehemu ndogo tu ya jambo hili, kuona baadhi ya mambo ya nje. Wazaliwa Wangu wa kwanza watakapojitokeza, basi Nitawaruhusu kuona kila kitu na kuelewa kila kitu. Kila mmoja atashawishika moyoni mwake na katika maneno yake. Nitawafanya msemi kwa sauti ili mnishuhudie, mnisifu milele, na mnitukuze milele. Hili haliepukiki na haliwezi kubadilishwa na yeyote. Watu hawawezi kuwazia jambo hili, sembuse kuliadini.

Wale ambao ni wazaliwa Wangu wa kwanza wanaendelea kuwa dhahiri kuhusu maono hayo, upendo wao Kwangu unazidi kuwa mwingi. (Huu si upendo wa mahaba, ambao ni Shetani kunishawishi, jambo linalohitaji kutambuliwa. Kwa hiyo zamani Nilinena kuwa kulikuwa na watu waliojigamba mbele Yangu. Watu wa aina hii ni vikaragosi wa Shetani, wakiadini kuwa Ningevisiwa na sura zao. Hawana haya! Mafidhuli duni!) Hata hivyo, watu wasiokuwa wazaliwa wa kwanza, kupitia katika maneno haya ambayo Nimezungumza katika kipindi hiki, wamezidi kutokuwa dhahiri kuhusu maono hayo na wamepoteza imani kwa mtu Niliye. Baadaye hatua kwa hatua wanakuwa wasiojali hadi hatimaye wanaanguka. Hawa watu hawawezi kujisaidia. Hili ndilo lengo la mambo Ninayoyasema wakati huu, kila mtu anapaswa kuona haya (Nikizungumza na wazaliwa Wangu wa kwanza), na kupitia kwa matamshi na matendo Yangu, watazame maajabu Yangu. Mbona inasemwa kuwa Mimi ni Mfalme wa Amani, Baba wa Milele, kuwa Mimi ni wa Ajabu, kuwa Mimi ni Mshauri? Haitoshi kabisa kufafanua jambo hili kutoka kwa utambulisho Wangu, matamshi Yangu, ama kutoka kwa yale Ninayofanya: Hata haistahili kutajwa. Sababu ya kuniita Mfalme wa Amani ni uwezo Wangu wa kuwakamilisha wazaliwa wa kwanza, hukumu Yangu kwa Shetani, na baraka zisizo na kifani ambazo Nimewatunuku wazaliwa wa kwanza. Hiyo ni kusema, ni wazaliwa wa kwanza pekee ndio wanaostahili kuniita Mfalme wa Amani, kwa kuwa Ninawapenda wazaliwa Wangu wa kwanza, na wasifu “Mfalme wa Amani” unafaa kutoka kwa vinywa vyao. Kwao, Mimi ni Mfalme wa Amani. Kwa wanangu na watu Wangu, Ninaitwa Baba wa Milele. Kwa sababu ya uwepo wa wazaliwa Wangu wa kwanza, kwa sababu wazaliwa Wangu wa kwanza wanaweza kushikilia nguvu ya ufalme pamoja

nami na kuyatawala mataifa yote na watu wote (wana na watu), kwa hiyo, wana na watu wanapaswa kuniita Baba wa Milele, kumaanisha Mungu Mwenyewe, aliye juu ya wazaliwa wa kwanza. Mimi ni wa Ajabu kwa wale wasiokuwa wana, watu na wazaliwa wa kwanza. Kwa sababu ya ajabu ya kazi Yangu, wasioamini hawawezi kuniona kamwe (kwa maana Nimeyafunika macho yao), na hawawezi kuona kazi Yangu vyema kabisa, kwa hivyo kwao Mimi ni wa Ajabu. Kwa mapepo wote na kwa Shetani Mimi ni Mshauri kwa sababu yote Niyafanyayo yanawatia aibu, na yote Nifanyayo ni kwa ajili ya wazaliwa Wangu wa kwanza. Kila hatua Yangu huenda taratibu na Ninapata ushindi kwa kila hatua. Zaidi ya hayo, Ninaweza kuitambua mipango yote ya Shetani na kutumia mipango yake kunitumikia, Nikimfanya kuwa chombo cha kutumikia makusudi Yangu kutoka kwa upande hasi. Hii ndiyo maana ya Mimi kuwa Mshauri, ambayo hakuna anaweza kubadilisha na hakuna anayeweza kuelewa kabisa. Lakini kuhusu nafsi Yangu, Mimi ni Mfalme wa Amani, pamoja na Baba wa Milele, na vile vile Mshauri na wa Ajabu. Hakuna kitu katika mambo haya ambayo si kweli. Ni ukweli usioplingwa na usiobadilika!

Nina mengi sana ya kusema, hayafananishwi kabisa. Kwa hiyo, Nawahitaji muwe na subira na kungoja. Chochote mfanyacho, msifanye kutokana na msukumo fulani wa kuondoka. Kwa sababu mlichokielewa siku za nyuma kimepitwa na wakati leo, hakitumiki tena, na mambo ya sasa ni wakati wa mabadiliko—kama mpito kati ya nasaba za wafalme, kwa hiyo Nawahitaji mbadili mawazo yenu na mtupe fikira zenu za kale. Hii ndiyo maana ya kweli ya “kuvalia joho takatifu la haki”. Ni Mimi pekee Ninayeweza kufafanua maneno Yangu mwenyewe, na ni Mimi pekee Ninayejua Ninayojiandaa kufanya. Kwa hiyo, ni maneno Yangu pekee yasiyo na najisi, ni yale Ninayokusudia kabisa, na kwa hiyo ni kuvalia joho takatifu la haki. Ufahamu wa akili ya binadamu ni mawazo tu; ufahamu wao ni wenye najisi na hauwezi kutimiza makusudi Yangu. Kwa hiyo Mimi mwenyewe Ninanena, na Mimi mwenyewe Ninaeleza, na hii ndiyo maana iliyokusudiwa ya “Ninaifanya kazi mwenyewe.” Ni sehemu muhimu ya mpango Wangu wa usimamizi, na ni sharti watu wote wanitukuze na kunisifu. Kuhusu kuelewa maneno Yangu, Sijawahi kuwapa watu uwezo huo na hawana ustadi wa hayo kamwe. Hii ni mojawapo ya mbinu Zangu za kumdhaliisha ibilisi. (Iwapo watu wangeelewa matamshi Yangu na wangepewe kuchunguza makusudi Yangu katika kila hatua, basi Shetani angewamiliki watu wakati wowote, na hivyo watu wangenigeuka na kufanya iwe vigumu Kwangu kutimiza lengo Langu la kuwateua wazaliwa wa kwanza. Kama Ningelewa kila siri, na mtu Niliye angeweza kunena matamko ambayo hakuna yeyote angeweza kuelewa, Mimi, pia ningeweza kumilikiwa na Shetani. Hii ndiyo sababu Nikiwa katika mwili Mimi si wa mwujiza kabisa.) Lazima kila mtu afahamu vizuri umuhimu wa maneno haya na kufanya mambo akifuata uongozi Wangu. Msijaribu ninyi wenyewe kufahamu maneno na mafundisho ya dini ya kina.

Sura ya 102

Nimeongea hadi kwa kiwango fulani na kufanya kazi hadi kwa kiwango fulani; ninyi nyote mnapaswa kuelewa mapenzi Yangu na kwa viwango tofauti muweze kuzingatia mzigo Wangu. Sasa ndicho kipindi muhimu kutoka katika mwili kuingia katika dunia ya roho, na ninyi ndio watangulizi kwa kutagaa enzi, watu wa ulimwengu wanaovuka ulimwengu na miisho ya dunia. Ninyi ni wapendwa Wangu zaidi; ninyi ndio Ninaowapenda. Inaweza kusemwa kwamba Sina wapendwa wengine ila ninyi, kwa sababu jitihada Yangu yote ya bidii imekuwa kwa ajili yenu— inaweza kuwa kwamba hamjui hilo? Kwa nini Niumbe vitu vyote? Kwa nini Nidhibiti vitu vyote ili kuwatumikia? Haya yote ni maonyesho ya upendo Wangu kwenu. Milima na vitu vyote milimani, dunia na vitu vyote duniani vinanisifu na kunitukuza kwa sababu Nimewapata ninyi. Kweli, kila kitu kimefanywa, na aidha, kila kitu kimefanyika kikamilifu. Mmekuwa na ushuhuda mkubwa sana kwa ajili Yangu na kufedhehesha ibilisi na Shetani kwa ajili Yangu. Watu, mambo, na vitu vyote nje Yangu vinatii mamlaka Yangu, na vyote, kwa sababu ya ukamilisho wa mpango Wangu wa usimamizi, vinafuata aina yao (Watu Wangu ni Wangu, na aina ya Shetani wote wanaenda kwa ziwa la moto—wanaenda kwa shimo lisilo na mwisho, ambapo watalia milele na kuangamia daima). Ninapozungumza kuhusu “kuangamia” na “kutoka wakati huo kuendelea kuchukua roho, nafsi na miili yao,” Ninarejelea kuwakabidhi kwa Shetani na kuwaruhusu kukanyagwa. Kwa maneno mengine, wote wasio wa nyumba Yangu watakuwa walengwa wa maandamizi na hawatakuwepo tena. Hili silo, kama wanavyofikiri watu, kwamba wataondoka. Na pia inaweza kusemwa kwamba kila kitu nje ya Mimi, kwa maoni Yangu, hakipo, ambayo ndiyo maana ya kweli ya kuangamia milele. Kwa macho ya wanadamu wanaonekana kuwepo bado, lakini katika maoni Yangu wamekuwa bure na wataangamia milele. (Mkazo uko kwa yeyote ambaye Sifanyii kazi tena na ambaye yuko nje ya Mimi.) Kwa wanadamu, bila kujali jinsi wanavyofikiri, hawawezi kuelewa hili, na bila kujali jinsi wanavyoona, hawawezi kulipenya. Hakuna mtu anayeweza kuelewa kwa wazi isipokuwa Nimpe nuru, Nimpe mwangaza, na kulionyesha kwa wazi. Aidha, watu wote watakuwa na wasiwasi zaidi na zaidi kulihusu, watahisi watupu hata zaidi, na watahisi kwa kuongeza kwamba hakuna njia ya kufuata—wao karibu ni kama wafu. Sasa hivi watu wengi (kumaanisha watu wote isipokuwa wazaliwa wa kwanza) wako katika hali hii. Nasema mambo haya kwa wazi sana na watu hawa hawana mjibizo mdogo na bado wanajali kuhusu raha zao za kimwili—wanakula na kisha kulala; wanalala na kisha wanakula, na hawatafakari maneno Yangu. Hata kama wamechangamshwa, itakuwa kwa muda tu, na baadaye watabaki vile vile walivyokuwa, wasibadilike kabisa, kana kwamba hawakunisikiza hata kidogo. Hawa ndio mfano hasa wa binadamu wasiojali wajibu ambao hawana mizigo—wasio na kazi dhahiri kabisa. Baadaye, Nitawatelekeza mmoja mmoja. Msijali! Nitawarudisha mmoja mmoja kwenye shimo lisilo na

mwisho. Roho Mtakatifu hajawahi kuwashughulikia watu kama hawa, na kila kitu waanachokifanya kinatokana na uwezo walioupokea. Ninapozungumza kuhusu hizi nyezo, Namaanisha kwamba huyu ni mtu asiye na uzima, ambaye ni mtendaji huduma Wangu. Simtaki yeyote kati yao na Nitawaondoa (lakini sasa hivi bado ana manufaa kiasi). Ninyi ambao ni watendaji huduma, sikizeni! Usifikiri kwamba Mimi kukutumia kunamaanisha kwamba Ninakupendelea. Si rahisi hivyo. Kama unataka Nikupendelea, lazima uwe mtu Nitakayemwidhinisha na lazima uwe mtu ambaye Nitamkamilisha binafsi. Huyu ni aina ya mtu ambaye Ninampenda. Hata kama watu wanasema Nimekosea, Sitawahi kuvunja ahadi. Unajua? Wale wanaotoa huduma ni ng'ombe na farasi. Wanawezaje kuwa wazaliwa Wangu wa kwanza? Hilo halitakuwa upuuzi? Huo hautakuwa ukiukaji wa sheria za asili? Yeyote aliye na uzima Wangu, ubora Wangu, wao ndio wazaliwa Wangu wa kwanza. Hili ni jambo la busara—hakuna mtu anayeweza kulikana. Lazima liwe hivyo, vinginevyo hakungekuwa na mtu ambaye angeweza kufanya wajibu huo, hakuna mtu ambaye angeweza kuchukua nafasi yake. Hili silo jambo la kutendewa kulingana na hisia, kwa kuwa Mimi ni Mungu Mwenyewe mwenye haki; Mimi ndiye Mungu mtakatifu Mwenyewe; Mimi ni Mungu mwenye uadhama, asiyekosewa Mwenyewe!

Yote ambayo hayawezekani kwa wanadamu yanaenda taratibu na kwa uhuru Kwangu. Hakuna anayeweza kulikomesha na hakuna mtu anayeweza kulibadili. Dunia kubwa kama hii yote iko mikononi Mwangu, sembuse Shetani mdogo ibilisi. Isingekuwa kwa sababu ya mpango Wangu wa usimamizi, na isingekuwa kwa sababu ya wazaliwa Wangu wa kwanza, Ngingekuwa nimeiharibu kitambo enzi hii nzee, ovu na zinzi ambayo imeenea harufu mbaya ya kifo. Lakini Natenda kwa utaratibu na Sizungumzi juu juu. Punde Ninapoongea litakamilishwa; hata kama hili halingekuwa hivyo, kuna kipengele cha hekima Yangu, ambacho kitakamilisha kila kitu kwa ajili Yangu na kufungulia matendo Yangu njia. Kwa kuwa maneno Yangu ni hekima Yangu; maneno Yangu ni kila kitu. Watu wanakosa kuyaelewa kimsingi na hawawezi kuyafahamu. Mara nyingi Ninarejelea “ziwa la moto.” Hili linamaanisha nini? Linatofautiana vipi na ziwa la moto na kibiriti? Ziwa la moto na kibiriti linarejelea ushawishi wa Shetani, na ziwa la moto linarejelea dunia nzima chini ya miliki ya Shetani. Kila mtu duniani ni wenye uelekeo wa kutolewa kafara katika ziwa la moto (yaani, wanazidi kuwa wapotovu na, upotovu wao unapofika kiwango fulani, wataangamizwa na Mimi mmoja mmoja, ambalo ni rahisi Kwangu kufanya kwa neno Langu moja pekee). Kadiri ghadhabu Yangu ilivyo kubwa, ndivyo moto mkali unavyokuwa mkubwa zaidi kotekote katika ziwa la moto. Hili linarejelea watu kuwa waovu zaidi na zaidi. Wakati huu ambapo ghadhabu Yangu inaripuka ndio pia utakuwa wakati ambapo ziwa la moto linalipuka; yaani, utakuwa wakati ambapo ulimwengu dunia mzima unaangamia. Siku hiyo ufalme Wangu utapatikana kikamilifu duniani na maisha mapya

yataanza. Hiki ni kitu ambacho kitatimizwa karibuni. Kwa kuwa Ninazungumza, kila kitu kitatimizwa papo hapo. Huo ndio mtazamo wa binadamu wa suala hilo, lakini katika mtazamo Wangu vitu vimekamilishwa mapema kwa sababu Kwangu kila kitu ni rahisi. Nasema na kinafanywa; Nasema na kinaanzishwa.

Kila siku mnakula maneno Yangu; mnafurahia wingi ulio katika hekalu Langu; mnakunywa maji kutoka kwa mto Wangu wa uzima; mnachuma tunda kutoka mti Wangu wa uhai. Basi, wingi katika hekalu Langu ni nini? Maji ya mto Wangu wa uzima ni nini? Mti wa uzima ni nini? Tunda la mti wa uzima ni nini? Virai hivi vya kawaida havieleweki hata hivyo kwa binadamu wote, ambao wamechanganyikiwa wote, wakivisema kwa njia isiyopaswa, wakivitumia kwa kutojali, na kuvitumia bila mpango maalum. Wengi katika hekalu haumaanishi maneno ambayo Nimezungumza au neema ambayo Nimewapa. Kwa hivyo, hata hivyo, unamaanisha nini? Tangu nyakati za zamani hakujawahi kuwa na mtu yeyote ambaye ana bahati kufurahia wingi katika hekalu Langu. Ni katika siku za mwisho tu, miongoni mwa wazaliwa Wangu wa kwanza, ndipo watu wanaweza kuona wingi katika hekalu Langu ni nini. “Hekalu” linalozungumziwa katika “wingi katika hekalu Langu” ni nafsi Yangu, likirejelea Mlima Sayuni, makao Yangu. Bila ruhusa Yangu hakuna mtu anayeweza kuliingia au kuliondoka. Je, “wingi” huu unamaanisha nini? Wengi unamaanisha baraka za kutawala pamoja na Mimi katika mwili. Kuzungumza kwa jumla, hili linamaanisha baraka za wazaliwa wa kwanza kutawala na Mimi katika mwili, na hili si gumu kuelewa. Maji ya mto wa uzima una maana mbili: Kwa upande mmoja unarejelea maji hai yanayotiririka kutoka kwa nafsi Yangu ya ndani sana, yaani, kila neno linalotoka katika kinywa Changu. Kwa upande mwingine, unarejelea hekima na maarifa ya matendo Yangu, na vile vile kile Nilicho na ninacho. Katika maneno Yangu kuna siri nyingi, zilizofichwa (kwamba siri hazifichwi tena kunazungumziwa kinyume na zamani, lakini kukilinganishwa na ufunuo wa umma katika siku ijayo, bado zimefichwa. Hapa, “kufichwa” si kamili, badala yake linategemea uhusiano), ambayo ni kusema kwamba maji ya mto wa uzima yanatiririka wakati wote. Ndani Yangu kuna hekima isiyo na kikomo, na watu hawawezi kuelewa kabisa kile Nilicho na ninacho hata kidogo; yaani, maji ya mto wa uzima yanatiririka milele. Katika mtazamo wa binadamu kuna aina nyingi za miti yakinifu, lakini hakuna mtu ambaye amewahi kuona mti wa uzima. Hata hivyo, licha ya kuona leo, watu bado hawaitambui—na bado hata wanazungumza kuhusu kula kutoka kwenye mti wa uzima. Hakika huu ni upuuzi kweli! Wangekula kwa mti huu bila mpango! Kwa nini Nasema leo watu wanauona lakini hawaitambui? Kwa nini Nasema hivyo? Je, unaelewa maana ya maneno Yangu? Mungu wa vitendo Mwenyewe wa leo ni mtu Niliye, na Yeye ndiye mti wa uzima. Usitumie dhana za binadamu kunipima—kutoka nje Sifanani na mti, lakini unajua kwamba Mimi ndio mti wa uzima? Kila tendo Langu, usemi na tabia Yangu, ni tunda la mti wa uzima, na ni nafsi Yangu—hayo ndiyo ambayo wazaliwa Wangu wa kwanza

wanapaswa kula, kwa hivyo hatimaye ni Mimi na wazaliwa Wangu wa kwanza pekee ndio tutakuwa sawa hasa. Wataweza kuishi kwa kunidhihirisha na wataweza kunishuhudia. (Haya ni mambo yanayofanyika baada ya sisi kuingia katika dunia ya roho. Ni katika mwili tu ndiyo tunaweza kuwa sawa kabisa; katika nyama tunaweza kuwa takribani sawa, lakini bado tuna aina zetu wenyewe).

Sionyeshi tu nguvu Yangu katika wazaliwa Wangu wa kwanza pekee, lakini pia Nitaonyesha nguvu Yangu kwa uongozi wa wazaliwa Wangu wa kwanza wa mataifa yote na watu wote. Hii ni hatua ya kazi Yangu. Sasa ndio wakati wa maana, na sasa ni kipindi muhimu hata zaidi. Wakati ambapo kila kitu kinakamilishwa, mtaona ni nini ambacho mikono Yangu inafanyia kazi, na mtaona Ninavyopanga na Ninavyosimamia, lakini hili si jambo lisilo yakini. Kulingana na elimumwendo ya kila nchi duniani, si tofauti sana; ni jambo ambalo watu hawawezi kulifikiria, na aidha, jambo ambalo hawawezi kuliona mbele. Ni lazima msiwe wazembe au wenye upurukushani hata kidogo ili msikose fursa ya kubarikiwa na kupewa zawadi. Matarajio ya ufalme yanaonekana na dunia nzima inakufa polepole. Kutoka kwa shimo lisilo na mwisho na kutoka kwa ziwa la moto na kibiriti kunatokea sauti kubwa za milio, zikiwaogofya watu na kuwafanya kuhisi kuogopa na kuaibika. Yeyote anayechaguliwa kwa jina Langu na kisha kuondolewa atakuwa katika shimo lisilo na mwisho. Kwa hivyo Nimesema nyakati nyingi, Nitarusha walengwa wa kuangamizwa ndani ya shimo lisilo na mwisho. Wakati ambapo dunia yote imeharibiwa kila kitu ambacho kimeharibiwa kitaenda katika ziwa la moto na kibiriti—yaani, kitahamishwa kutoka katika ziwa la moto hadi kwenye ziwa la moto na kibiriti. Wakati huo kila mtu atakuwa ameamuliwa kuangamizwa milele (kumaanisha wote ambao wako nje ya Mimi) au kupata uzima wa milele (kumaanisha wale wote ambao wako ndani ya Mimi). Wakati huo Mimi na wazaliwa Wangu wa kwanza tutaibuka kutoka kwa ufalme na kuingia katika uzima. Hili ni jambo ambalo litatimizwa baadaye, na hata Nikiwaambia sasa, hamtaelewa. Mnaweza tu kufuata mwongozo Wangu, mtembee katika mwanga Wangu, kuambatana nami katika upendo Wangu, kufurahia nami katika nyumba Yangu, kutawala nami katika ufalme Wangu, na kuwa na kutawala nami juu ya mataifa yote na watu wote katika mamlaka Yangu. Kile ambacho Nimesema hapo juu ni baraka zisizoisha ambazo Ninawapa.

Sura ya 103

Sauti ya mngurumo inatoka, ikiutetemesha ulimwengu mzima, ikiwahanikiza watu, na kuwafanya wachelewe kukwepa, na wengine wanauawa, baadhi wanaangamizwa, na wengine wanahukumiwa. Kweli ni kioja ambacho hakuna yeyote amewahi kukiona awali. Sikiliza kwa makini, milio ya radi inafuatana na sauti za kuomboleza, na sauti hii inatoka kuzimu, sauti hii inatoka jahanamu. Ni sauti yenye uchungu ya wale wana wa uasi ambao wamehukumiwa nami.

Wale wasiosikiza kile Ninachosema na hawatendi maneno Yangu wanahukumiwa vikali na kupokea laana ya ghadhabu Yangu. Sauti Yangu ni hukumu na ghadhabu, nami si mpole kwa yeyote na simwonei mtu yeyote huruma, kwa kuwa Mimi ni Mungu mwenye haki Mwenyewe, na Mimi ni mwenye ghadhabu, Nina kuchoma, utakaso, na maangamizo. Ndani Yangu, hakuna kitu kilichofichika, au chenye mhemuko, lakini badala yake, kila kitu kiko wazi, chenye haki, na kisicho na upendeleo. Kwa sababu wazaliwa Wangu wa kwanza tayari wako nami katika kiti cha enzi, wakitawala mataifa yote na watu wote, yale mambo na watu walio dhalimu na waovu wanaanza kuhukumiwa. Nitawafanyia uchunguzi mmoja baada ya mwingine, bila kukosa kitu chochote, Nikiwafichua kabisa. Kwa kuwa hukumu Yangu imefichuliwa kikamilifu na imefunguliwa kikamilifu, na hakuna chochote ambacho kimebakizwa; Nitatupa chochote kisichokubaliana na mapenzi Yangu na kukisababisha kiangamie kuzimu milele; Nitakisababisha kiungue kuzimu milele. Hii ni haki Yangu; huu ni uaminifu Wangu. Hakuna mtu anayeweza kubadilisha hili, na lazima kinitii.

Watu wengi hupuuza maneno Yangu na kufikiri maneno ni maneno tu na ukweli ni ukweli. Wao ni wajinga! Hawajui kwamba Mimi ni Mungu mwaminifu Mwenyewe? Maneno Yangu na ukweli hutokea sawia—si hii kwa hakika ni kweli? Watu hawaelewi maneno Yangu kabisa, na wale tu ambao wamepata nuru wanaweza kuelewa kweli—huu ni ukweli. Mara tu watu wanapoonaa maneno Yangu wanaogopa sana, wakijificha kila mahali, sembuse wakati hukumu Yangu inaposhuka. Nilipoumba vitu vyote, Ninapouharibu ulimwengu, na Ninapowakamilisha wazaliwa wa kwanza—mambo haya yote yanatimizwa kwa neno moja kutoka katika kinywa Changu. Hii ni kwa maana neno Langu lenyewe ni mamlaka; hilo nihukumu. Inaweza kusemwa kuwa mtu Niliye ni hukumu na uadhama; huu ni ukweli usiobadilika. Huu ni upande mmoja wa amri Zangu za utawala; njia moja Kwangu kuwahukumu watu. Machoni Pangu, watu wote, masuala yote, na vitu vyote—vitu vyote kabisa—viko mikononi Mwangu na viko chini ya hukumu Yangu, hakuna mtu na hakuna kitu chochote kinachothubutu kutenda bila mpango na kwa makusudi, na yote lazima yatimizwe kwa mujibu wa maneno Ninayonena. Kutoka katika mawazo ya binadamu kila mtu anaamini maneno ya mtu Niliye. Wakati Roho Wangu anatoa sauti, watu wanakuwa na wasiwasi. Hawajui kudura Yangu kabisa, nao wananingizia. Ninakuambia! Yeyote anayeyatilia shaka maneno Yangu, yeyote anayeyadharau maneno Yangu, hawa ndio watakaoangamizwa, ni wana wa kudumu wa kuangamia kabisa. Kutokana na hili inaweza kuonekana kuwa kuna wachache sana ambao ni wazaliwa wa kwanza, kwa sababu hii ndiyo mbinu Yangu ya kufanya kazi. Kama Nilivyosema, Sijitahidi kufanya lolote, lakini badala yake Mimi hutumia maneno Yangu tu kutimiza kila kitu. Hii, basi, ndipo ambapo kudura Yangu huwa. Katika maneno Yangu hakuna mtu anayeweza kupata chanzo na madhumuni ya hotuba Yangu. Watu hawawezi kutimiza hili, na wanaweza tu kutenda kulingana na mwongozo Wangu,

na wanaweza tu kufanya kila kitu kulingana na mapenzi Yangu kufuatana na haki Yangu, ili familia Yangu iwe na haki na amani, ikiishi milele, thabiti na imara milele.

Hukumu Yangu inamjia kila mtu, amri Zangu za utawala zinamgusa kila mtu, na maneno Yangu na nafsi Yangu vinafichuliwa kwa kila mtu. Huu ndio wakati wa kazi kuu ya Roho Wangu (wakati huu wale watakaobarikiwa na wale watakaopitia taabu wanabainishwa). Mara tu maneno Yangu yatakapotamkwa, Nimewabainisha wale watakaobarikiwa na wale watakaopitia taabu. Yote ni dhahiri nami Ninaweza kuyaona mara moja. (Yanasemwa kuhusu ubinadamu Wangu, kwa hiyo hayahitilafiani na majaaliwa na uteuzi Wangu.) Ninatembatembea hapa na pale milimani na mito na vitu vyote, anga ya ulimwengu, Nikichunguza kila mahali na kutakasa kila mahali, ili yale maeneo yasiyo safi na zile nchi zilizochangamana zote zitakoma kuwepo nazo zitateketea kabisa kwa sababu ya maneno Yangu. Kwangu, kila kitu ni rahisi. Ikiwa wakati huu ungekuwa wakati ambao Niliamua kabla kuiangamiza dunia, Ningeimeza kwa neno moja, lakini sasa si wakati. Lazima kila kitu kiwe tayari kabla Yangu kufanya kazi hii, ili visiuvuruge mpango Wangu na kuingilia usimamizi Wangu. Ninajua jinsi ya kufanya hivyo kwa busara: Nina hekima Yangu nami Nina mpango Wangu wenyewe. Watu hawapaswi kufanya lolote—jihadhari usiuawe kwa mkono Wangu; tayari hii inagusa amri Zangu za utawala. Kutokana na hili mtu anaweza kuona ukali wa amri Zangu za utawala, na mtu anaweza kuona kanuni za amri Zangu za utawala, ikiwa ni pamoja na vipengele viwili: kwa upande mmoja Ninawaua wote wasiokubaliana na mapenzi Yangu na ambao wanazikosea amri Zangu za utawala; kwa upande mwingine, Nikiwa na ghadhabu Ninawalaani wote wanaozikosea amri Zangu za utawala. Vipengele hivi viwili ni muhimu navyo ni kanuni zenye mamlaka ya uamuzi za amri Zangu za utawala. Kila mtu hutendewa kulingana na kanuni hizi mbili, bila hisia, bila kujali jinsi watu walivyo waaminifu. Hii inatosha kuonyesha haki Yangu na inatosha kuonyesha uadhama Wangu na ghadhabu Yangu, ambayo itaviteketeza vitu vyote ya kidunia, vitu vyote vya kidunia, na vitu vyote ambavyo havikubaliani na mapenzi Yangu. Katika maneno Yangu kuna siri zilizofichwa, na katika maneno Yangu pia kuna siri zilizofichuliwa, hivyo katika dhana ya binadamu, katika akili ya binadamu, maneno Yangu hayaeleweki milele na moyo Wangu haueleweki milele. Kwa maneno mengine, lazima Niwaondolee wanadamu dhana na kufikiria kwao. Hiki ni kipengee muhimu zaidi cha mpango Wangu wa usimamizi. Lazima Nifanye hivi ili Niwapate wazaliwa Wangu wa kwanza na ili Niyakamilishe mambo ambayo Nataka kufanya.

Maafa ya dunia yanakua makubwa zaidi siku baada ya siku, na kati ya familia Yangu misiba mikuu inakuwa yenye nguvu hata zaidi. Kwa kweli watu hawana mahali pa kujificha nao wana aibu na hawawezi kuonyesha nyuso zao. Kwa sababu mpito ni sasa, hakuna mtu anayejua wapi atapitia hatua yake inayofuata. Itakuwa dhahiri tu baada ya hukumu Yangu. Kumbuka! Hizi ndizo hatua za kazi Yangu, na ndiyo njia ambayo kwayo Mimi hufanya kazi. Nitawaliwaza

wazaliwa Wangu wa kwanza wote mmoja mmoja, na kuwatia moyo hatua baada ya hatua; na kwa watendaji huduma wote, Nitawaondosha na kuwatelekeza mmoja baada ya mwingine. Hii ni sehemu moja ya mpango Wangu wa usimamizi. Baada ya watendaji-huduma wote kufichuliwa, wazaliwa Wangu wa kwanza watafichuliwa pia. (Kwangu, jambo hili ni rahisi sana. Baada ya wao kusikia maneno Yangu, watendaji-huduma wote hao wataondoka polepole chini ya hukumu na tishio la maneno Yangu, na wale watakaobaki watakuwa tu wazaliwa Wangu wa kwanza. Hili si jambo la hiari nalo si jambo ambalo ridhaa ya mwanadamu inaweza kubadilisha, bali ni Roho Wangu anayefanya kazi binafsi.) Hili si tukio la mbali, nanyi mnapaswa kulielewa kwa kiasi fulani kutoka ndani ya awamu hii ya kazi Yangu na maneno Yangu. Halieleweki kwa watu kwa nini Niseme mengi sana na hayatabiriki. Ninawazungumzia wazaliwa Wangu wa kwanza kwa sauti ya faraja, huruma, na upendo (kwa sababu daima Mimi huwapa nuru watu hawa na Sitawaacha, kwa kuwa Nimewajaalia), huku Nikiwatendea kwa hukumu kali watu wengine isipokuwa wazaliwa Wangu wa kwanza, kwa vitisho, na kwa kuwaogofya, Nikiwafanya kuwa na hofu daima kiasi kwamba wamesisimka daima. Wakati hali inapoendelea hadi kiwango fulani, basi watakimbia kutoka katika hali hii (Nitakapoiangamiza dunia, watu hawa watakuwa katika kuzimu), lakini hawatawahi kuepuka mkono Wangu wa hukumu, na hawataepuka hali hii kamwe. Hii, basi, ni hukumu yao; huku ndiko kuadibu kwao. Siku ambayo wageni watawasili Nitawafichua watu hawa mmoja baada ya mwingine. Hii ni hatua katika kazi Yangu. Sasa mnaelewa kwa nini Nilinena maneno hayo hapo awali? Kwa maoni Yangu jambo ambalo halijakamilishwa pia ni jambo ambalo limekamilishwa, lakini jambo lililokamilishwa si lazima liwe jambo ambalo limetimizwa, kwa sababu Nina hekima Yangu, nami Nina njia Yangu ya kufanya kazi, ambayo haieleweki kwa wanadamu kabisa. Wakati Nimepata matokeo katika hatua hii (wakati Nimewafichua wabaya wote wanaonipinga Mimi), kisha Nitaanza hatua inayofuata, kwa sababu mapenzi Yangu hayapingwi na hakuna mtu anayethubutu kuuzuia mpango Wangu wa usimamizi na hakuna kitu kinachothubutu kuweka vikwazo—wanapaswa kuondoka wanipishe! Wana wa joka kubwa nyekundu, sikilizeni! Nilitoka Sayuni na kuwa mwili katika ulimwengu ili Niwapate wazaliwa Wangu wa kwanza, ili Nimdhalilishe baba yenu (hii inazilenga dhuria za joka kubwa nyekundu), ili kuwaunga mkono wazaliwa Wangu wa kwanza, na kusahihisha makosa waliyotendewa wazaliwa Wangu wa kwanza. Kwa hiyo msiwe wakatili tena; Nitawafanya wazaliwa Wangu wa kwanza wawashughulikie. Wakati uliopita wana Wangu walidhulumiwa na kukandamizwa, na kwa kuwa Baba hushika madaraka kwa ajili ya wana, wana Wangu watarudi katika kumbatio Langu la upendo, wasidhulumiwe na kukandamizwa tena. Mimi si dhalimu; hii inaonyesha haki Yangu, na kwa kweli ni "kuwapendwa Ninaowapenda na kuwachukia Ninaowachukia." Ikiwa mnasema Mimi ni mdhalimu, mnapaswa kuondoka haraka. Msiwe wapujufu na kudoea katika familia Yangu. Unapaswa kurudi nyumbani kwako haraka ili Nisilazimike kukuona tena. Kuzimu ni hatima yenu napo ni mahali ambapo

ninyi hupumzika. Mkiwa katika familia Yangu hakutakuwa na nafasi kwa ajili yenu kwa sababu ninyi ni wanyama wa kuchukua mizigo, ninyi ndizo zana ambazo Natumia. Nisipowatumia Nitawatupa ndani ya moto ili Niwateketeze. Hii ni amri Yangu ya utawala; lazima Niifanye hivi, na hii tu inaonyesha jinsi Ninavyofanya kazi na inaonyesha haki Yangu na uadhama Wangu. La muhimu zaidi ni kwamba njia hii pekee ndiyo inaweza kuwawezesha wazaliwa Wangu wa kwanza kutawala pamoja nami katika mamlaka.

Sura ya 104

Watu, matukio, na vitu vyote nje Yangu vitakufa na kuwakatika hali ya kutokuwepo, ilhali watu, matukio na vitu vyote vilivyo ndani Yangu vitapata kila kitu kutoka Kwangu na kuingia katika utukufu pamoja na Mimi, kuingia katika Mlima Wangu Sayuni, makazi Yangu, na kuishi pamoja kwa amani nami milele. Niliumba vitu vyote mwanzoni na Nitamaliza kazi Yangu mwishowe, na pia Nitatawala milele kama Mfalme. Katikati, pia Ninaongoza na kuutawala ulimwengu mzima. Hakuna anayeweza kuondoa mamlaka Yangu, kwani Mimi ni Mungu mmoja Mwenyewe, na pia Nina uwezo wa kupitisha mamlaka Yangu kwawazaliwa Wangu wa Kwanza, ili wazaliwa Wangu wa kwanza waweze kutawala kandokando Yangu. Hili lipo milele na haliwezi kubadilishwa kamwe. Hii ni amri Yangu ya utawala. (Mahali popote Ninapojadili amri Yangu ya utawala, Ninazungumzia kile kinachofanyika katika ufalme Wangu na kile kitakuwepo milele na hakiwezi kubadilishwa kamwe.) Lazima kila mtu aridhishwe kwa moyo wote, na lazima aone uwezo Wangu mkubwa ndani ya wale Ninaowapenda. Hakuna anayeweza kuliaibisha jina Langu—yeyote afanyaye hilo ni lazima aondoke hapa! Si kwamba Sina huruma, ila kwamba wewe ni mdhalimu. Iwapo utakiuka adabu Yangu basi Nitakushughulikia na kusababisha wewe kuangamia milele na milele. (Bila shaka, haya yote yamewalenga watu wasio wazaliwa Wangu wa kwanza.) Takataka kama hiyo hairuhusiwi katika nyumba Yangu, kwa hivyo harakisha na uondoke hapa! Usichelewe hata kwa dakika moja au kwa sekunde moja! Lazima ufanye Ninachosema, au sivyo Nitakuangamiza kwa neno moja. Ni heri usisite bado, ni heri usidanganye bado. Wale wanaobuni upuuzi mbele Yangu, wale wanaodanganya mbele Yangu—ondokeni haraka! Muda Wangu ni mchache kwa mambo kama hayo. (Ikifika wakati wa kufanya huduma watafanya huduma, na ikifika wakati wa kuondoka wataondoka. Nafanya mambo kwa hekima, bila kupoteza dakika au sekunde, hazipotezwi hata kidogo. Yote ni ya haki na sahihi kabisa.) Lakini kwa wazaliwa Wangu wa kwanza, Mimi ni mvumilivu bila kikomo nami Napenda hadi mwisho milele, Nikiwawezesha kufurahia baraka nyingi milele na maisha ya milele pamoja nami, na kwa sasa kutovumilia kipingamizi au hukumu tena. (Hii inahusu wakati mnaanza kufurahia baraka.) Hii ni baraka na ahadi isiyo na kikomo kwa wazaliwa Wangu wa kwanza Nilipoiumba dunia. Mnapaswa kuiona haki Yangu humo—Napenda wale ambao Nimewajaalia, Nawachukia wale ambao Nimewaacha na kuwaondoa, milele na milele.

Kama wazaliwa Wangu wa kwanza, nyote mnapaswa kushikilia wajibu wenu wenyewe na kusimama katika nafasi zenu, muwe malimbuko yaliyonyakuliwa mbele Yangu na kukubali uchunguzi Wangu binafsi, ili mweze kuishi kwa kudhihirisha taswira Yangu tukufu na mwanga wa utukufu Wangu uweze kung'aa kupitia nyuso zenu, ili matamshi Yangu yaweze kuenezwa kupitia vinywa vyenu, ili kwamba ufalme Wangu uweze kutawaliwa na ninyi, na ili kwamba watu Wangu waweze kutawaliwa na ninyi. Hapa Nataja “malimbuko” na pia neno kama “kunyakuliwa.” Malimbuko ni nini? Katika dhana za watu, wanafikiri ni kundi la kwanza la watu wanaonyakuliwa, au kwamba inarejelea washindi au watu ambao ni wazaliwa wa kwanza. Haya yote ni uwongo na ufahamu wa uwongo wa maneno Yangu. Malimbuko ni watu ambao wamepokea ufunuo kutoka Kwangu na kupata mamlaka kutoka Kwangu. Hii inayodaiwa kuwa “malimbuko” inahusu kumilikiwa na Mimi, kujaaliwa na kuchaguliwa na Mimi. “Malimbuko” halimaanishi ya kwanza katika mfuatano. “Malimbuko” si jambo yakinifu machoni pa mwanadamu. Inayodaiwa kuwa “malimbuko” inahusu kitu kinachotoa harufu nzuri (hii ni maana ya ishara), yaani, wale wanaoweza kuishi kwa kunidhihirisha, kunidhihirisha, na kuishi nami milele. Ninapozungumza kuhusu “matunda” Ninarejelea wana na watu Wangu wote, ilhali malimbuko linarejelea wazaliwa wa kwanza ambao watatawala kama wafalme kandokando Yangu. Hivyo, “malimbuko” linapaswa kuelezwa kama kuwa na mamlaka. Hiyo ni maana ya kweli. “Kunyakuliwa” si kuchukuliwa kutoka mahali pa chini kwenda mahali pa juu jinsi watu wanaweza kufikiria; hiyo ni fikira potovu sana. “Kunyakuliwa” kunaashiria kujaaliwa Kwangu halafu kuchagua. Hii inawalenga wale wote ambao Nimewaamua kabla na kuwachagua. Wale wote wataonyakuliwa ni watu waliopata hadhi ya wazaliwa wa kwanza, au wana, auwale ambao ni watu wa Mungu. Hili halilingani kabisa na mawazo ya watu. Wale walio na sehemu katika nyumba Yangu katika siku zijazo wote ni watu ambao wamenyakuliwa mbele Yangu. Hii ni kweli kabisa, haibadiliki kamwe, na haiwezi kukataliwa na mtu yeyote. Hili ni jibu la mapigo dhidi ya Shetani. Mtu yeyote Niliyemwamua kabla atanyakuliwa mbele Yangu.

Mtu anaelezaje “tarumbeta takatifu”? Ni nini ufahamu wenu wa hili? Mbona inasemwa kuwa takatifu na iliyopigwa tayari? Hili linapaswa kuelezwa kutoka kwa hatua za kazi Yangu na kueleweka kutoka kwa mbinu ya kazi Yangu. Wakati ambapo hukumu Yangu inatangazwa kwa umma ni wakati tabia Yangu inafichuliwa kwa mataifa na watu wote. Huo ndio wakati tarumbeta takatifu inapigwa. Yaani kwamba Nasema mara nyingi kwamba tabia Yangu ni takatifu na isiyokosewa, ambayo ndiyo maana “takatifu” inatumika kuelezea “tarumbeta.” Inaweza kuonekana kutoka kwa hili kwamba “tarumbeta” inarejelea tabia Yangu na inawakilisha kile Nilicho na Nilicho nacho. Inaweza pia kusemwa kwamba hukumu Yangu inaendelea kila siku, ghadhabu Yangu inatolewa kila siku, laana Yangu inafikia kila kitu kisicholingana na tabia Yangu kila siku. Basi inaweza kusemwa kwamba wakati hukumu Yangu huanza ni wakati

tarumbeta takatifu inapigwa, na inapigwa kila siku, bila kukoma kwa muda au bila kukoma kwa dakika au sekunde. Kuanzia sasa na kuendelea, tarumbeta takatifu itatoa sauti kubwa zaidi na zaidi sawa na kushuka kwa taratibu kwa maafa makuu. Yaani, pamoja na ufunuo wa hukumu Yangu ya haki, tabia Yangu itakuwa wazi zaidi na zaidi, na kile Nilicho na Nilicho nacho kitaongezwa ndani ya wazaliwa Wangu wa kwanza zaidi na zaidi. Hii ni mbinu ya kazi Yangu ya baadaye; kwa upande mmoja kuruzuku na kuwaokoa wale Ninaowapenda, na kwa upande mwingine kutumia maneno Yangu kuwafichua wale wote Ninaowadharau. Kumbuka! Hii ni mbinu ya kazi Yangu, hatua za kazi Yangu, ambayo ni kweli kabisa. Hii imepangwa na Mimi tangu uumbaji na haiwezi kubadilishwa na yeyote.

Bado kuna sehemu nyingi za maneno Yangu ambazo ni ngumu kwa watu kuelewa, hivyo basi Nimeendeleza zaidi njia Yangu ya kusema na mbinu Zangu za kufichua siri. Kwa maneno mengine, njia Yangu ya kusema inabadilika na kuwa nzuri zaidi kila siku, kwa mtindo na mbinu tofauti kila siku. Hizi ndizo hatua za kazi Yangu na haziwezi kubadilishwa na mtu yeyote. Watu wanaweza tu kusema na kutenda kulingana na kile Ninachosema. Huu ndio ukweli hasa. Nimefanya mipango ya kufaa kwa nafsi Yangu na mwili Wangu. Ndani ya kila hatua na kitendo cha ubinadamu Wangu kuna kipengele cha hekima ya uungu Wangu. (Kwa kuwa binadamu hawana hekima hata kidogo, kusema kwamba wazaliwa wa kwanza wana hekima Yangu kunarejelea wazaliwa wa kwanza kuwa na tabia Yangu takatifu ndani yao.) Wazaliwa wa kwanza wanapofanya mambo ya kipumbavu, ni kwa sababu bado mna chembechembe za binadamu ndani yenu. Hivyo basi ni lazima muondoe upumbavu kama huo wa binadamu na kufanya kile Ninachokipenda na kukataa kile Ninachokichukia. Yeyote anayetoka Kwangu lazima arudi ndani Yangu. Yeyote anayezaliwa kutoka Kwangu lazima arudi ndani ya utukufu Wangu. Wale Ninaowachukia lazima waachwe na kuondolewa kutoka Kwangu, mmoja mmoja. Hizi ndizo hatua za kazi Yangu; huu ni usimamizi Wangu, na ni mpango wa uumbaji Wangu wa miaka elfu sita. Wale wote Ninaowaacha wanapaswa kunitii na kuniacha kwa utii. Wale wote Ninaowapenda, kwa sababu ya baraka Nilizowapa, wanapaswa kunisifu ili jina Langu liweze kuwa tukufu hata zaidi, na mwanga mtukufu uweze kuongezwa kwa uso Wangu mtukufu, ili kwamba waweze kujaa hekima Yangu katika utukufu Wangu, na kulitukuza jina Langu hata zaidi katika mwanga Wangu mtakatifu!

Sura ya 105

Kwa sababu ya kanuni za maneno Yangu, kwa sababu ya utaratibu wa kazi Yangu, watu hunikana; hili ndilo kusudi Langu la kuzungumza kwa muda mrefu (imezungumzwa kuhusu wazao wote wa joka kubwa jekundu). Ni njia ya hekima ya kazi Yangu; ni hukumu Yangu ya joka kubwa jekundu; huu ni mkakati Wangu, hakuna mtu hata mmoja anayeweza kuelewa

kikamilifu. Katika kila kipindi muhimu, yaani, katika kila awamu ya mpito ya mpango Wangu wa usimamizi, baadhi ya watu lazima waondolewe; wanaondolewa kulingana na utaratibu wa kazi Yangu. Hii pekee ndiyo njia ya kazi ya mpango Wangu wote wa usimamizi. Baada ya kuwatupa nje, mmoja baada ya mwingine, watu Ninaotaka kuwaondoa, kisha Ninaanza hatua inayofuata ya kazi Yangu. Hata hivyo, wakati huu wa kuondosha ni wakati wa mwisho (ndani ya makanisa ya China), na pia ni wakati ambapo idadi kubwa ya watu itaondolewa katika awamu ya mpito tangu uumbaji wa ulimwengu. Katika historia yote, kila wakati ambapo watu wameondolewa kumekuwa na sehemu iliyoachwa ili kutoa huduma kwa kazi ya baadaye, lakini wakati huu sio sawa na hapo awali; ni nyumbufu na safi, ni muhimu zaidi na kamilifu zaidi kuliko nyakati zote. Hata ingawa baada ya kusoma maneno Yangu, watu wengi hujaribu kuyalazimishia shaka kutoka akilini mwao, lakini mwishoni wao hawawezi kuyashinda, na hatimaye wanaanguka katika mapambano yao. Hili sio juu ya mwanadamu kuamua, kwa sababu wale ambao Nimewajaalia hawawezi kutoroka, na wale ambao Sijawajaalia Ninaweza kuwadharau tu. Ni wale ambao Ninawaangalia kwa fadhila pekee ndio ambao Ninawapenda, vinginevyo, hakuna hata mtu mmoja anayeweza kuondoka na kuingia kwa hiari katika ufalme Wangu; huu ndio utawala Wangu mkali, na huu pekee ndio ushahidi wenye nguvu na udhihirisho kamili wa kutekeleza amri Zangu za utawala. Hakika hili si suala la kuwa na moyo wenye ari tu. Kwa nini Nimesema Shetani ni dhaifu na aliyeanguka? Mara ya kwanza alikuwa na nguvu, lakini yuko katika mikono Yangu; Nikimwambia alale chini, ni lazima alale; Nikimwambia ainuke ili kunitolea huduma, ni lazima ainuke na kutoa huduma Kwangu vizuri. Siyo kwamba Shetani yuko radhi kufanya haya, ni kwamba fimbo Yangu ya chuma humtawala Shetani, na ni wakati huo pekee ndipo anaridhika moyoni na kwa neno. Amri Zangu za utawala humwongoza, Nina uwezo Wangu, na hivyo hana budi ila kuridhika kabisa, lazima apondwe chini ya kiti Changu cha miguu, bila dalili ya upinzani. Hapo zamani wakati ambapo alikuwa akiwahudumia wana Wangu, alikuwa fidhuli kupita kiasi na aliwadhulumu wana Wangu kwa hiari, akitumai kwa njia hiyo kuniaibisha Mimi, akisema kuwa Sina uwezo. Kipofu kweli! Nitakukanyaga hadi ufe! Wewe thubutu tu kuwa nduli tena! Wewe thubutu tu kuwatendea wana Wangu kwa kutojali kwa baridi tena! Kadiri watu wanavyokuwa waaminifu zaidi, na kadiri wanavyozidi kusikiliza maneno Yangu na kunitii, ndivyo unavyozidi kuwadhalimu, na ndivyo unavyozidi kuwatenga (hii ina maana kuwasajili watu, kuwaunganisha pamoja). Sasa siku zako za ukatili ziko mwishoni, kidogo kidogo Ninalipiza kisasi kwako, na Sitakuachilia kwa urahisi hata kidogo. Sasa sio wewe—Shetani—ambaye umechukua mamlaka; badala yake Nimechukua mamlaka hayo tena, na wakati wa kuwaita wana Wangu kukushughulikia umewadia. Ni lazima utii, na usiwe na upinzani hata kidogo. Bila kujali jinsi ulivyokuwa na mwenendo mzuri mbele Yangu hapo zamani, hilo halitakusaidia leo. Kama wewe si mmoja wa wale Ninaowapenda, basi Sikutaki. Mmoja zaidi ya idadi hiyo haikubaliki, lazima iwe nambari Niliyoamua kabla; mmoja

chini ya hiyo ni mbaya zaidi. Shetani, usiwe mdakizi! Je, inaweza kuwa kwamba Sina hakika katika moyo Wangu kuhusu yule ambaye Ninampenda na ambaye Ninamchukia? Je, Ninahitaji kukumbushwa nawe? Shetani anaweza kuzaa wana Wangu? Wote ni wa upuuzi! Wote ni duni! Nitawatupa kabisa na kikamilifu, hakuna hata mmoja anayetakikana, wote lazima waondoke! Mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita umefika mwisho, Kazi Yangu imekamilika na ni lazima Niliondoe kundi hili la wanyama na wenye tabia mbaya na wakatili!

Wale wanaoamini maneno Yangu na kutekeleza maneno Yangu lazima wawe wale Ninaowapenda, Sitamwacha hata mmoja, hakuna hata mmoja atakayeachwa huru, hivyo wale ambao ni wana wazaliwa wa kwanza hawana haja ya kuwa na wasiwasi. Kwa kuwa imetolewa na Mimi, hakuna mtu anayeweza kuichukua, na Sina budi kuwakirimu wale Ninaowabariki. Wale ambao Ninawakubali (kabla ya uumbaji wa ulimwengu), Ninawabariki (leo). Hivi ndivyo Ninavyofanya kazi, pia ndiyo kanuni kuu ya kila kifungu cha amri Zangu za utawala, na hakuna mtu anayeweza kubadilisha hili; neno moja zaidi haliwezi kuongezwa, wala sentensi moja zaidi, na hata zaidi neno moja haliwezi kuachwa, wala sentensi moja. Hapo zamani mara nyingi Nilisema kuwa nafsi Yangu inaonekana kwenu; hivyo basi nafsi Yangu ni nini, na huonekana vipi? Je, ina maana Mimi Mwenyewe tu? Je, ina maana ya kila sentensi ambayo Ninasema tu? Vipengele hivi viwili, huku vikiwa vya msingi, vinachukua tu sehemu ndogo, yaani, hivyo sio maelezo kamili ya nafsi Yangu. Nafsi Yangu inajumuisha Mimi Mwenyewe, maneno Yangu, na pia matendo Yangu, lakini ufafanuzi halisi ni kwamba Mimi na wana Wangu wazaliwa wa kwanza tu nafsi Yangu. Yaani, kikundi cha wanadamu wa shirika la Ukristo, ambao hutawala na wana mamlaka, ni nafsi Yangu. Kwa hivyo, kila mmoja wa wana wa kwanza ni muhimu, ni sehemu ya nafsi Yangu, na tangu sasa Nasisitiza kwamba idadi ya watu haiwezi kuwa zaidi kwa mmoja (ikidhalilisha jina Langu), wala, hata muhimu zaidi, haiwezi kuwa ndogo kwa mmoja (haliwezi kuwa dhihirisho Langu kamili), na Nasisitiza tena na tena kwamba wana wa kwanza ni wapendwa Wangu, tunu Yangu, udhihirisho wa mpango Wangu wa usimamizi wa miaka elfu sita; ni wazaliwa wa kwanza pekee wanaoweza kuwa dhihirisho Langu timilifu na kamili, Mimi Mwenyewe pekee ndiye ninayeweza kuwa onyesho kamili la nafsi Yangu; pamoja tu na wana wa kwanza ndipo Mimi mwenyewe naweza kusemekana kuwa ni onyesho timilifu na kamili. Hivyo, Ninaweka madai makali kwa wana Wangu wa kwanza, bila kusamehe chochote, na kukata na kuua wale wote walio tofauti na wana Wangu wa kwanza tena na tena; hiki ndicho kiini cha yote ambayo Nimeyasema, ndilo lengo kuu la yote ambayo Nimeyasema. Zaidi ya hayo, mara nyingi Mimi husisitiza kuwa lazima wawe wale waliodhinishwa na Mimi, wale ambao Nimewachagua binafsi tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Hivyo, sasa ni ipi namna ya kueleza “kuonekana”? Je, ni wakati wa kuingia katika ulimwengu wa kiroho? Watu wengi wanaamini kwamba ni wakati ambapo Mimi Mwenyewe Nilitiwa mafuta, au wakati ambapo

waliniona Mimi Mwenyewe; yote haya ni uongo, hata hayakaribii ukweli. “Kuonekana” kwa mujibu wa maana yake ya asili si vigumu kuelewa kabisa, lakini kuelewa kulingana na nia Yangu ni vigumu sana. Inaweza kusemwa hivi: Wakati ambapo niliwaumba binadamu, Nilikuwa nikiweka ubora Wangu katika kundi hili la watu Niliowapenda, na kundi hili la watu lilikuwa nafsi Yangu. Ili kuieleza kwa njia nyingine, nafsi Yangu ilikuwa tayari imeonekana wakati huo. Siyo kwamba nafsi Yangu ilionekana baada ya jina hili kupokewa, bali badala yake ilionekana baada ya kuliambia kabla kundi hili la watu, kwa sababu lina ubora Wangu (asili yao haibadiliki, wao bado ni sehemu ya nafsi Yangu). Kwa hivyo, nafsi Yangu, tangu uumbaji wa ulimwengu mpaka siku ya sasa, imeonekana daima. Katika dhana za watu, wengi wanaamini kwamba Mimi Mwenyewe ndimi nafsi Yangu, ambayo sivyo kabisa; hayo yote ni mawazo ya watu, fikra za watu. Kama nafsi Yangu ya mwili pekee ingekuwa nafsi Yangu, basi hiyo haingeweza kutosha kumtia aibu Shetani. Isingeweza kulitukuza jina Langu, na kwa kweli ingekuwa na athari za kinyume, na hivyo kuliaibisha jina Langu, na kuwa alama ya Shetani kuliletea aibu jina Langu katika enzi zote. Mimi ni Mungu mwenye hekima Mwenyewe, na siwezi kamwe kufanya jambo la upumbavu kama hilo.

Kazi Yangu lazima iwe na matokeo, hata zaidi ni lazima Niseme maneno kwa utaratibu; Maneno Yangu yote na matamshi Yangu yanasemwa kwa kufuata Roho Wangu, na mimi husema kulingana na yote ambayo Roho Wangu hufanya. Kwa hivyo wote wanapaswa, kwa njia ya maneno Yangu, kuhisi Roho Wangu, kuona ni nini hasa ambacho Roho Wangu anafanya, kuona ni nini hasa Ninachotaka kufanya, kuona njia Yangu ya kufanya kazi kulingana na maneno Yangu, na kuona kanuni za mpango Wangu mzima wa usimamizi ni zipi. Mimi hutazama taswira nzima ya ulimwengu: Kila mtu, kila tukio, na kila mahali, vyote viko chini ya utawala Wangu. Hakuna mtu anayeweza kukiuka mpango Wangu; wote husonga mbele hatua kwa hatua kwa utaratibu ambao Nimeagiza. Huu ni uwezo Wangu, ni pale ambapo hekima ya kusimamia mpango Wangu wote upo. Hakuna anayeweza kuelewa kikamilifu, hakuna anayeweza kusema waziwazi. Yote hufanywa na Mimi binafsi, na kudhibitiwa na Mimi pekee. Yote hufanywa na Mimi binafsi, na kudhibitiwa na Mimi pekee.

Sura ya 106

Wale wasioyajua maneno Yangu, wale wasioujua ubinadamu Wangu wa kawaida, na wale wanaokataa uungu Wangu wote wataangamizwa hadi wasikuwepo. Hakuna atakayeachiliwa kutokana na hili, na wote lazima wafikie kipengele hiki kwa njia ya kuridhisha, kwa sababu ni amri Yangu ya utawala, na hiki ndicho kifungu cha uzito zaidi cha kuweka fanya kwa matendo. Wale wasioyajua maneno Yangu ni wale ambao wamesikiliza yale ambayo Nimesema wazi, ilhali bado hawayajui, kwa maneno mengine wale ambao hawaelewi masuala ya kiroho (kwa

kuwa Sijaumba sehemu hii ya mwili kwa ajili ya wanadamu, Sihitaji mengi kutoka kwao; Nahitaji tu kwamba wasikilize maneno Yangu na kisha wayaweke katika matendo). Wao sio watu wa nyumba Yangu, sio wa aina moja na Mimi; ni wa ufalme wa Shetani. Kwa hivyo simtaki hata mmoja wa hao watu wasioelewa masuala ya kiroho. Hapo awali, mlifikiria Nilikuwa nimezidi; leo mtaelewa. Wanyama watawezaje kuzungumza na Mungu? Huo si upuuzi? Wale wasiojua ubinadamu Wangu wa kawaida ni wale ambao wanatumia fikira zao wenyewe kupima Nifanyacho katika ubinadamu Wangu. Badala ya utiifu, wao, kwa macho yao ya kimwili, wanajaribu kunikosa Mimi mambo madogo madogo. Pengine Nimenena bure? Nilisema ubinadamu Wangu wa kawaida ni sehemu Yangu ya lazima, Mungu mkamilifu Mwenyewe, na hii ni njia halisi ambayo ubinadamu Wangu wa kawaida na uungu kamili unafanya kazi kwa pamoja: Wakati ambapo vitu Nifanyavyo kupitia kwa ubinadamu Wangu wa kawaida havipatani na dhana za mwanadamu, wale wanaonikataa na wale wasiolingana na Mimi wanafichuliwa. Baada ya haya, uungu Wangu kamili unanena kupitia katika ubinadamu, na kwa njia hii, Nimewashughulikia watu wengine kwa namna hii. Kama huelewi Ninachofanya lakini hata hivyo unatii, mtu wa aina hii Simshutumu, ila Nampa nuru. Huyu ni aina ya mtu Ninayempenda, na kwa sababu ya utiifu wako Nakupa nuru. Wale wanaokataa uungu Wangu ni pamoja na wale ambao hawajui maneno Yangu, wale ambao hawalingani na ubinadamu Wangu wa kawaida, na wale ambao hawapendi Ninachofanya katika uungu (kwa mfano, kukasirika Kwangu au ujenzi wa kanisa na kadhalika). Hayo yote ni maonyesho ya kukataa uungu Wangu. Lakini kuna kitu kimoja Ninachosisitiza na kila mmoja wenu lazima awe makini: Watu ambao hawalingani na mtu ambaye Niliye leo wanapinga uungu Wangu. Mbona Naendelea kusema kuwa mtu amabye Niliye ni Mungu Mwenyewe mkamilifu? Tabia ya mtu amabaye Niliye ni inajumuisha ujumla wa tabia takatifu; usitumie fikira za wanadamu kunipima Mimi. Hata sasa, watu wengi bado wanasema kuwa Nina ubinadamu wa kawaida na hivyo vitu Nifanyavyo sivyo sahihi vyote. Watu hawa—je, hamjitafutii kufa? Hawajui neno hata moja ya yale Ninayosema, na ni ukoo wa vipofu kabisa, wazawa wa joka kuu jekundu. Nitawaambia kila mmoja mara nyingine (na Sitasema tena baada ya hapo, yeyote akikiuka hili tena, kwa hakika atalaaniwa): Maneno Yangu, kicheko Changu, kula Kwangu, kuishi Kwangu, usemi Wangu na tabia yote yanafanywa na Mimi—Mungu Mwenyewe, na hakuna dalili hata kidogo ya mwanadamu iliyochanganyika ndani, hakuna! Hakuna kabisa! Kila mtu anapaswa kukoma kucheza michezo yake ya akili, koma na hesabu zako ndogo ndogo. Kadiri unavyoendelea na hili zaidi ndivyo utakavyoangamia zaidi. Sikia ushauri Wangu!

Kila mara Naangalia ndani zaidi ya moyo wa kila mmoja, Naangalia kila moja ya neno na tendo lake, na naona kwa wazi, mmoja baada ya mwingine, wale Ninaowapenda na wale Nisiowapenda. Hili ni jambo ambalo watu hawawezi kufikiria, na hata zaidi, jambo ambalo watu

hawawezi kutimiza. Nimesema mengi sana na Nimefanya vitu vingi sana; ni nani angeweza kunena wazi juu ya ni nini malengo Yangu kwa matamshi Yangu, na kwa kazi Yangu? Hakuna anayeweza kunena kuyahusu kwa wazi. Baada ya hii, Sitanena zaidi; kwa upande moja hii itawaangamiza watu wote ambao Siwapendi, na kwa upande mwingine, itawafanya mteseke zaidi kidogo kuhusu hii, ili kwa mara nyingine mpate kupitia ufufuo kutoka kwa wafu lakini na ukali zaidi. Hili haliwezi kuamuliwa na watu, na hakuna anayeweza kuliepa. Hata kama unajua kuhusu haya sasa, wakati utakapofika bado hutaweza kuepuka mateso haya, kwa sababu hivi ndivyo Nafanya kazi. Lazima Nifanye kazi hivi ili Nifikie malengo Yangu, na ili Niache mapenzi Yangu yatimike kwenu. Hii ndiyo sababu yanaitwa “mateso ya mwisho ambayo lazima upitie.” Mwili wenu hautateseka tena baadaye, kwa sababu joka kuu jekundu litakuwa limeangamizwa na Mimi, na halitathubutu kuleta ghasia tena. Hii ndiyo hatua ya mwisho kabla ya kuingia katika mwili; ni hatua ya mpito. Lakini msigope, bila shaka Nitawaongoza kwa mgogoro baada ya mgogoro. Amini kuwa Mimi ni Mungu mwenye haki Mwenyewe. Kile ambacho Nimesema kitatimizwa kwa hakika. Mimi ni Mungu mwaminifu Mwenyewe. Mataifa yote, nchi zote, na madhehebu yote yanarejea Kwangu na kukusanyika kwa kiti Changu cha enzi. Hii ni nguvu Yangu kubwa, na Nitamhukumu kila mwana muasi, Nikiwatupa katika ziwa la moto na kiberiti, bila ubaguzi wowote, wote lazima wajiondoe. Hii ndiyo hatua ya mwisho ya mpango Wangu wa usimamizi, na wakati ambapo hii itakamilika, Nitaingia katika mapumziko, kwa sababu kila kitu kitakuwa kimefanyika, na mpango Wangu wa usimamizi utakuwa umefika mwisho.

Kwa sababu kasi ya kazi Yangu imeongezeka (ingawa moyo Wangu hauna wasiwasi), Nafichua maneno Yangu kwenu kila siku, Nafunua mafumbo Niliyo nayo kwenu kila siku, ili mfuata kwa karibu nyayo Zangu. (Hii ni busara Yangu, kutumia maneno Yangu kuwakamilisha watu, lakini pia kuwaangamiza watu. Wote wanasoma maneno Yangu, na wanaweza kutenda kulingana na mapenzi Yangu katika maneno Yangu. Wale walio hasi watakuwa hasi, wale ambao wanafaa kufichuliwa wataonyesha tabia zao za kweli, wanaokataa watakataa, na wale wanaonipenda kwa uaminifu watakuwa waaminifu hata zaidi. Kwa hivyo, wote wanaweza kufuata nyayo Zangu. Hali kadhaa Nilizoeleza zote ni mbinu za jinsi Ninavyofanya kazi na ni malengo Ninayotaka kufikia). Hapo awali Nimesema: Haijalishi Ninavyowaongoza, mnafaa kufuata kwa njia iyo hiyo; chochote Ninachowaambia, mnafaa kusikia. Nilimaanisha nini Nikisema hili? Je mnajua? Lengo na umuhimu wa neno Langu ni nini? Je mnaelewa? Ni watu wangapi wanaweza kueleza hili kwa ufasaha kikamilifu? Ninaposema “Haijalishi Ninavyowaongoza, mnafaa kutafutata kwa njia iyo hiyo,” Simaanishi tu uongozi Wangu Ninaowapa kama mtu Niliye; aidha Ninaashiria maneno Ninenayo na njia Ninayopitia. Leo, neno hili limekamilika kweli. Baada tu ya kunena maneno Yangu, aina yote ya nyuso za kipepo

inawekwa wazi mbele ya mwanga wa uwepo Wangu, ili muweze kuiona yote kwa wazi. Neno hili Langu silo tu tangazo kwa Shetani, ila ni kuaminiwa kwa ninyi wote. Wengi wenu mnapuza neno hili, mkiliamini kuwa ni kuaminiwa kwa ninyi, lakini hamgundui kuwa hili ni neno la hukumu, neno ambalo linabeba mamlaka. Lengo la maneno Yangu ni kumwamuru Shetani kunifanyia Mimi huduma vizuri na kunitii kabisa. Katika mafumbo Niliyofichua hapo zamani, bado kuna mengi ambayo hamwelewi bado, kwa hivyo baadaye Nitawafichulia mengi zaidi, ili muweze kuwa na uelewa wazi na mkamilifu kabisa.

Majanga yanapokuja, kila mtu anahofu. Watu wote hulia kwa huzuni na kuhisi chuki ya mambo maovu waliyotenda zamani, lakini kufikia wakati huo watakuwa wamechelewa sana, kwani hii ni enzi ya ghadhabu. Sio wakati wa kuokoa watu na kutoa neema, ila ni wakati wa kuwaondoa watendaji huduma wote na kuwacha wana Wangu kutawala kwa niaba Yangu. Kwa kweli hii ni tofauti na zamani, na haijawahi kutokea kutoka uumbaji wa dunia. Kwa sababu Nimeumba dunia mara moja, Nitaangamiza dunia mara moja, na yale ambayo Nimeamua kabla hayawezi kubadilishwa na yeyote. Maneno haya mawili “ushirika wa wanadamu Wakristo” na “ushirika wa wanadamu wote wapya” yalitajwa mara nyingi awali. Yanafaa kuelezwa vipi? Je, ushirika wa wanadamu Wakristo unaashiria wazaliwa wa kwanza? Je, ushirika wa wanadamu wote wapya unaashiria pia wazaliwa wa kwanza? Hapana, watu hawajitafsiri barabara. Kwa sababu dhana za binadamu zinaweza tu kuelewa vitu kwa kiwango hiki, Nitaweka hili wazi hapa na sasa kwenu. Ushirika wa wanadamu Wakristo na ushirika wa wanadamu wote wapya sio sawa; maana yao ni tofauti. Ingawa kwa maneno haya mawili hayana tofauti sana, na yanaweza kuonekana kuwa kitu kimoja, hali ya kweli ni kinyume kabisa. Ushirika wa wanadamu Wakristo unaashiria akina nani hasa? Ama wao wanaashiria nini? Tukiongelea wanadamu Wakristo, kila mmoja atanifikiria Mimi. Wote hawajakosea kabisa kufanya hivi. Zaidi, katika dhana za wanadamu, neno “wanadamu” bila shaka linaashiria wanadamu, na hakuna mtu hata mmoja anayeweza kulishirikisha na kitu kingine. Tunapoongelea “ushirika,” watu wanaweza kufikiria huu ni mkusanyiko wa watu wengi na karibu ni kitengo kimoja, kwa hivyo unaitwa ushirika. Hapa inaweza kuonekana kuwa akili za mwanadamu ni sahili sana, na haziwezi kuelewa kusudi Langu kabisa. Sasa, Nitaanza rasmi kushiriki kuhusu ushirika wa wanadamu Wakristo ni akina nani (lakini kila mmoja lazima aweke kando dhana zake, la sivyo hakuna atakayeweza kuelewa, na hata kama Ningeleeza neno hilo, watu hawangeliamini, wala kulielewa): Baada tu ya maneno Yangu kunenwa, wazaliwa Wangu wa kwanza wote wataweza kutenda kulingana na mapenzi Yangu, na kuonyesha mapenzi Yangu, ili kwamba wawe ni wa moyo mmoja na wa kunena jambo moja. Wanapohukumu mataifa yote na watu wote, wataweza kutekeleza haki Yangu, na kutekeleza amri Zangu za utawala; wao ni maonyesho Yangu, na ni udhihirisho Wangu. Hivyo, inaweza kusemekana kuwa ushirika wa wanadamu Wakristo ni tendo la hakika la wana

wazaliwa wa kwanza kutekeleza amri Zangu za utawala, wao ni mamlaka katika mikono ya wazaliwa wa kwanza; na hili lote linahusiana na Kristo, ndio sababu ya neno wanadamu Wakristo. Zaidi, wazaliwa wa kwaza wote wanaweza kutenda kulingana na mapenzi Yangu, kwa hivyo Ninatumia neno ushirika. Ushirika wa wanadamu wote wapya unamaanisha watu wote walio katika jina Langu, kwa maneno mengine, wazaliwa Wangu wa kwanza, wana Wangu, na watu Wangu. “Wapya” linaashiria jina Langu. Kwa sababu wako katika jina Langu (Jina Langu linabeba kila kitu, na ni jipya milele na halizeeki kamwe, halibadilishwi na mwanadamu), na wao watabaki hai milele baadaye, wao ni watu wapya wa ulimwengu. “Ushirika” hapa linahusu idadi ya watu, na sio sawa na hali ya awali. Wakati neno Langu linanewa, wote lazima waliadini. Usiwe na shaka. Ondoa dhana zako za kibinadamu na fikira za kibinadamu. Mchakato Wangu wa sasa wa kufichua mafumbo ni hasa mchakato wa kutoa dhana za kibinadamu na fikira (kwa sababu watu hutumia dhana zao kunipima Mimi na kupima Ninachosema, Ninatumia mafumbo Yangu Mwenyewe yaliyofichuliwa kutoa dhana za kibinadamu na kutoa fikira za kibinadamu). Kazi hii itakamilika hivi karibuni. Mafumbo Yangu yanapofichuliwa kwa hatua fulani, watu hawatakuwa na mchakato ya mawazo kuhusu maneno Yangu na watakoma kutumia dhana zao za kibinadamu kunipima Mimi. Kile wanachofikiria kila siku, Nitafichua, na Nitalipiza kisasi. Katika hatua fulani, watu hawatafikiria tena, vichwa vyao vitakuwa tupu bila mawazo yoyote, na watatii maneno Yangu kabisa, na hapo ndipo utaingia katika ulimwengu wa kiroho. Hii ni hatua katika kazi Yangu kabla ya kuwaruhusu mwingie katika ulimwengu wa kiroho. Lazima mwondoe dhana za kibinadamu kabla ya kuweza kuwa mtakatifu na bila dosari na kuingia katika ulimwengu wa kiroho, na hii ndiyo maana asili ya “Mimi ni mwili mtakatifu wa kiroho.” Lakini lazima mtende kulingana na hatua Zangu, na kabla ya ninyi kutambua, wakati Wangu utakuja.

Sura ya 107

Wakati maneno Yangu yanafikia kiwango fulani cha ukali, watu wengi huondoka kwa sababu yake—na ni katika wakati huu hasa ndipo wazaliwa Wangu wa kwanza wanafichuliwa. Nimesema kuwa Sitafanya lolote, lakini Nitatumia tu maneno Yangu kutimiza mambo yote. Ninatumia maneno Yangu kuwaangamiza wote ambao Ninawachukia, na pia Ninatumia maneno Yangu kuwakamilisha wazaliwa Wangu wa kwanza. (Maneno Yangu yatakaponenwa, ngurumo saba zitatoa sauti, na wakati huo wazaliwa Wangu wa kwanza pamoja na Mimi tutabadili sura na kuingia katika ulimwengu wa kiroho.) Niliposema Roho Wangu hufanya kazi binafsi, Nilichomaanisha ni kuwa maneno Yangu hutimiza yote, na kupitia kwa hili mtu anaweza kuona kwamba Mimi ni mwenyezi. Kwa hiyo, mtu anaweza kuona kwa uwazi mkubwa hata zaidi lengo na kusudi la kila moja ya sentensi Zangu. Nimesema awali, kila kitu Ninachosema ndani ya ubinadamu Wangu ni kipengele cha dhihirisho Langu. Kwa hiyo, wale watu ambao hawawezi

kuwa na uhakika na ambao hawaamini kweli kile Ninachosema ndani ya ubinadamu Wangu wa kawaida lazima waondolewe! Nimesisitiza tena na tena kwamba ubinadamu Wangu wa kawaida ni kipengele muhimu cha uungu Wangu kamili, ilhali watu wengi sana bado wanalenga uungu Wangu kamili huku wakupuuza ubinadamu Wangu. Wewe ni kipofu! Unasema kwamba Silingani na mawazo yako, na kwamba mwanadamu Niliye halingani na fikira yako ya alivyo Mungu. Je, watu hawa wanaweza kusalia katika ufalme Wangu? Nitakukanyaga chini ya miguu Yangu! Hebu thubutu tu kuniasi! Nakwambia uthubutu kuendelea na ukaidi kama huo! Tabasamu Yangu hairidhishi dhana unazoshikilia, usemi Wangu haukufurahishi, na matendo Yangu si yenye manufaa kwako, sivyo? Mambo haya yote yanapaswa kuwa kama uyapendavyo—je, hivyo ndivyo Mungu alivyo? Na watu hawa wanataka kusalia nyumbani Kwangu, na kupokea baraka katika ufalme Wangu? Je, si unaona njozi? Kungewezaje kuwa na jambo la ajabu kama hilo! Unataka kuniasi, ilhali bado upokee baraka kutoka Kwangu. Nakwambia: Haiwezekani! Wale ambao huingia katika ufalme Wangu na kupokea baraka lazima wawe watu ambao Ninawapenda, kama Nilivyosema mara nyingi. Kwa nini Ninasisitiza maneno haya? Najua na kuelewa kile ambacho kila mtu anafikiri moyoni mwake, Sihitaji kuonyesha mawazo yao yote. Sura zao za kweli zitafichuliwa kupitia kwa maneno Yangu ya hukumu na wote watalia kwa huzuni mbele ya kiti Changu cha hukumu. Huu ni ukweli dhahiri ambao hakuna anayeweza kubadilisha! Mwishowe, Nitawaamuru kuingia katika shimo lisilo na mwisho mmoja baada ya mwingine. Hii ni athari ya mwisho ya hukumu Yangu ya ibilisi Shetani. Lazima Nitumie hukumu na amri za utawala kumtendea kila mtu, na hii ndiyo mbinu Yangu ya kuadibu. Je! mna utambuzi wa kweli kuhusu jambo hili? Sihitaji kumpa Shetani sababu, Mimi hutumia tu fimbo Yangu ya chuma kumpiga mpaka afikie kiwango cha kukaribia kufa na kuomba msamaha kwa kurudia. Kwa hivyo, watu wanapasoma maneno Yangu ya hukumu, hawawezi kuyaelewa hata kwa kiwango kidogo, lakini kutoka kwa mtazamo Wangu, kila msitari na kila sentensi ni utekelezaji wa amri Zangu za utawala. Huu ni ukweli dhahiri.

Tangu leo Ninatoa hukumu, hii inahusisha kiti cha hukumu. Awali mmesema mara nyingi kuwa mtapokea hukumu mbele ya kiti cha Kristo. Mna ufahamu kuhusu hukumu, lakini hamwezi kuwazia kiti cha hukumu. Labda watu wengine wanafikiri kwamba kiti cha hukumu ni kitu cha kimwili, wanaweza kukifikiria kuwa meza kubwa, au labda kukifikiria kuwa kiti cha hukumu kama katika dunia ya kilimwengu. Bila shaka, katika ufafanuzi Wangu wakati huu, Sitakataa yale ambayo mmesema, lakini Kwangu, mambo yaliyomo katika mawazo ya watu bado yana maana yenye ishara. Hivyo ghuba kati ya mawazo ya watu na maana Yangu ya asili bado ni pana kama umbali kati ya mbinguni na dunia. Katika fikira za watu, kuna watu wengi wanaosujudu mbele ya kiti cha hukumu, wakilia kwa huzuni na kuomba msamaha. Huu tayari ni upeo wa mawazo ya binadamu na hakuna mtu anayeweza kufikiria chochote zaidi ya hayo. Kiti

cha hukumu ni nini basi? Kabla Nifichue siri, lazima mkanushe yote ambayo mmefikiri awali na ni wakati huo tu ndipo lengo Langu linaweza kufikiwa. Hii ndiyo njia ya pekee ambayo dhana na mawazo yenu katika eneo hili yanaweza kuondolewa. Lazima msikilize kwa makini nyakati zote Ninaponena. Sharti msiwe wazembe. Kiti Changu cha hukumu kimekuwa thabiti tangu uumbaji wa ulimwengu. Katika enzi na vizazi vilivyopita, watu wengi wamekufa mbele ya kiti Changu cha hukumu, na watu wengi wamefufuka mbele ya kiti hicho, wakiurudia uzima. Pia inaweza kusemwa kuwa tangu mwanzo hadi mwisho hukumu Yangu haikomi kamwe, na hivyo kiti Changu cha hukumu kipo daima. Kiti cha hukumu kinapotajwa, wanadamu wote wanakuwa na dalili ya hofu ndani yao. Bila shaka, kutokana na kile Nilichosema awali, hamjui kabisa kiti cha hukumu ni nini. Kiti cha hukumu na hukumu vinaishi pamoja kwa amani, lakini ni vifaa viwili tofauti. (Kifaa si kitu cha kimwili, lakini kinahusu maneno. Watu hawawezi kukiona kabisa.) Hukumu inahusu maneno Yangu. (Bila kujali kama ni makali au ya upole, yote yanajumuishwa katika hukumu Yangu. Hivyo, chochote Ninenacho kutoka kinywani Mwangu ni hukumu.) Awali, watu waliyagawanya maneno Yangu katika aina nyingi, ikiwa ni pamoja na maneno ya hukumu, maneno mapole, na maneno ambayo hutoa uhai. Leo, Nitawafanulia kuwa hukumu na maneno Yangu yameunganishwa moja kwa nyingine. Kwa maneno mengine, hukumu ni maneno Yangu, na maneno Yangu ni hukumu. Hampaswi kuvizungumzia vikiwa vimetengana. Katika mawazo ya watu, wanafikiri kwamba maneno makali ni hukumu, lakini watu wana ufahamu kiasi tu. Kila kitu Ninachosema ni hukumu. Mwanzo wa hukumu uliosema zamani unahusu Roho Wangu akianza kufanya kazi rasmi kila mahali na kutekeleza amri Zangu za utawala. Katika sentensi hii, “hukumu” inahusu ukweli halisi. Sasa Nitaeleza kiti cha hukumu: Kwa nini Ninasema kuwa kiti cha hukumu kipo milele hata milele na huenda na hukumu Yangu? Je, mnalielewa kutoka kwa ufafanuzi Wangu wa hukumu? Kiti cha hukumu kinarejelea mwanadamu Niliye. Milele hata milele, daima Mimi hueleza na kunena. Naishi milele, hivyo kiti Changu cha hukumu na hukumu Yangu vitaishi pamoja kwa amani milele. Lazima jambo hili liwe dhahiri sasa! Watu hunichukulia kama kitu katika mawazo yao, lakini kuhusu suala hili Siwalaumu na mimi Siwahukumu. Natamani tu kuwa mtakuwa na mioyo mitiifu na kukubali ufunuo Wangu, na kujua kutoka kwa ufunuo huo kwamba Mimi ndimi Mungu wa mambo yote Mwenyewe.

Maneno Yangu hayaeleweki na watu kabisa, haiwezekani kwao kupata nyayo Zangu, na haiwezekani kwao kuelewa mapenzi Yangu. Kwa hiyo, hali mliomo leo (kuweza kupokea ufunuo Wangu, kuelewa mapenzi Yangu kutoka ndani yake, na kufuata nyayo Zangu kupitia kwa ufunuo huo) ni matokeo ya vitendo Vyangu vya ajabu kabisa, neema Yangu na rehema Zangu. Siku moja, hata Nitawaruhusu muone hekima Yangu, muone yale Niliyoyatenda kwa mikono Yangu, na kuona ajabu ya kazi Yangu. Basi, mipangilio ya mpango Wangu wote wa

usimamizi itafichuliwa kabisa machoni penu. Kotekote katika ulimwenguni dunia wote na kila siku, kuna dhihirisho la vitendo Vyangu vya ajabu, na wote wanatoa huduma ili mpango Wangu wa usimamizi uweze kutimizwa. Hii itakapofichuliwa kabisa, mtaona ni aina gani ya watu Niliowapanga kutoa huduma, ni aina gani ya watu Nimewapanga kutimiza mapenzi Yangu, kile ambacho Nimetimiza kwa kumnyonya Shetani, kile ambacho Nimetimiza Mimi mwenyewe, ni aina gani ya watu wanaolia, ni aina gani ya watu wanaosaga meno yao, ni aina gani ya watu watakaoangamia, na ni aina gani ya watu watakaoteseka milele. Kwa kutaja “maangamizi”, Ninanena kuhusu wale ambao watatupwa katika ziwa la moto na kiberiti na watakaochomwa kabisa; kwa kutaja “kuteseka milele” Ninamaanisha wale ambao watatupwa katika shimo lisilo na mwisho kutesekea huko milele. Kwa hivyo, msifikirie visivyo kuwa maangamizi na kuteseka milele ni kitu kimoja; kinyume na hilo, mambo haya mawili ni tofauti kabisa. Watendaji huduma wanaoliacha jina Langu leo watateseka milele, na wale ambao si wa jina Langu wataenda kwa maangamizi. Hii ndiyo maana Ninasema wale wanaoteseka milele watanipa sifa za milele baada ya hukumu Yangu, lakini watu hao hawataepuka kuadibu Kwangu kamwe, watakubali utawala Wangu daima. Ndiyo maana Ninasema kwamba shimo lisilo na ni mkono ambao Ninatumia kuwaadibu watu. Pia Ninasema kwamba yote yako mikononi Mwangu. Ingawa Nimesema kwamba “shimo lisilo na mwisho” linahusu ushawishi wa Shetani, pia liko katika mikono Yangu ambayo Natumia kuwaadibu watu. Kwa hiyo, Ninaposema kuwa yote yako mikononi Mwangu, hakuna kweli kinzani. Maneno Yangu si ya kutoaminika. Hayo ni sahihi na yenye kueleweka. Si yaliyobuniwa au ya upuuzi, na kila mtu anapaswa kuamini maneno Yangu. Hapo baadaye, mtateseka kwa sababu ya hili. Kwa sababu ya maneno Yangu, watu wengi hukosa mhemuko, au hukata tamaa, au kusikitika, au hulia, au hutoa machozi. Kutakuwa na aina zote za kiitikio. Siku moja, wakati watu wote Ninaowachukia wataondoka, kazi Yangu itatimizwa. Hapo baadaye, watu wengi wataanguka kwa sababu ya wazaliwa wa kwanza, na mwishowe wataondoka hatua kwa hatua. Kwa maneno mengine, nyumba Yangu itakuwa takatifu hatua kwa hatua, na kila aina ya pepo wabaya watakimbia polepole kutoka upande Wangu, kimya, kwa unyenyekevu, na bila malalamiko yoyote. Baada ya hapo, wazaliwa Wangu wa kwanza watafichuliwa, nami Nitaanza hatua inayofuata ya kazi Yangu. Ni wakati huo tu ndipo wazaliwa wa kwanza watakuwa wafalme pamoja nami na kuutawala ulimwengu mzima. Hizi ndizo hatua za kazi Yangu, na zinafanyiza sehemu muhimu ya mpango Wangu wa usimamizi. Usikose kutilia maanani jambo hili, vinginevyo utakuwa umekosea.

Wakati ambapo maneno Yangu yatafichuliwa kwenu ni wakati ambapo Nitaanza kazi Yangu. Hakuna hata neno moja kati ya maneno Yangu ambayo halitatimizwa. Kwangu, siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. Je, mnalifikiriaje? Dhana yenu ya muda ni tofauti sana na Yangu, kwa sababu mimi huudhibiti ulimwengu dunia, na Mimi

hutimiza mambo yote. Kazi Yangu inafanyika kila siku, hatua kwa hatua, na kipindi kwa kipindi, na zaidi ya hayo kasi ya kazi Yangu haikomi hata kidogo, inaendelea kila wakati. Tangu kuumbwa kwa ulimwengu, maneno Yangu hayajakatizwa. Nimeendelea kunena na kueleza, hata leo, na haitabadilika katika siku za baadaye. Hata hivyo, muda Wangu unapangwa na kuratibiwa kwa uangalifu, na makini kabisa. Nitafanya Ninachohitaji kufanya wakati Ninahitaji kukifanya (na Mimi, wote wataachiliwa huru, wote watakuwa huru), na sikatizwi hata kidogo kuhusiana na hatua za kazi Yangu. Ninaweza kumpanga kila mtu nyumbani Kwangu, Ninaweza kumpanga kila mtu duniani, lakini Sina shughuli nyingi hata kidogo, kwa sababu Roho Wangu anafanya kazi, Roho Wangu hujaza kila mahali, kwa sababu Mimi ni Mungu wa pekee Mwenyewe na ulimwengu dunia wote uko mikononi Mwangu. Hivyo, mtu anaweza kuona kwamba Mimi ni mwenyezi, Mimi ni mwenye hekima na utukufu Wangu hujaza kila pembe ya ulimwengu.

Sura ya 108

Ndani Yangu, wote wanaweza kupata raha na wote wanaweza kuwa huru. Wale walio nje Yangu hawawezi kupata uhuru na furaha kwa sababu Roho Wangu hayuko pamoja na watu hawa. Watu hawa wanaitwa wafu wasio na roho. Nami Nawaita wale walio ndani Yangu watu walio hai wenye roho. Wao ni Wangu, na watarudi kwenye kiti Changu cha enzi. Wale ambao hutoa huduma na wale ambao ni wa ibilisi ni wafu wasio na roho, nao wanapaswa kuangamizwa hadi wawe katika hali ya kutokuwepo. Hii ni siri ya mpango Wangu wa usimamizi, na kitu ambacho wanadamu hawawezi kuelewa kuhusu mpango Wangu wa usimamizi, lakini pia Nimeliweka jambo hili hadharani kwa kila mtu. Wale ambao si Wangu wako kinyume Changu; wale ambao ni Wangu ni wale wanaolingana nami. Bila shaka hii ni kweli, na hii ndiyo kanuni ya hukumu Yangu kwa Shetani. Kila mtu anapaswa kujua kanuni hii ili aweze kuona haki na uadilifu Wangu—wale wote wanaotoka kwa Shetani watahukumiwa na kuchomwa na kugeuzwa majivu. Hii pia ni ghadhabu Yangu, na mtu anaweza kuona tabia Yangu zaidi. Kuanzia sasa na kuendelea, tabia Yangu itatangazwa waziwazi—itafichuliwa hatua kwa hatua kwa watu wote na mataifa yote, kwa dini zote, madhehebu yote, na watu wa kazi na viwango tofauti katika jamii. Hakuna kitu kitakachofichwa. Yote yatafichuliwa. Ni kwa sababu tabia Yangu na kanuni ya utendaji Wangu ni siri zilizofichwa kabisa kwa ajili ya wanadamu ambazo ni lazima Nifanye hivi (kwa namna kwamba wazaliwa wa kwanza hawatazikosea amri Zangu za utawala, na pia ili kutumia tabia Yangu iliyofichuliwa kuwahukumu watu wote na mataifa yote). Huu ni mpango Wangu wa usimamizi, na hizi ni hatua za kazi Yangu. Hakuna mtu atakayebadilisha jambo hilo kwa kupuuza. Tayari Nimeishi kwa kudhihirisha tabia kamili ya uungu Wangu katika ubinadamu Wangu, kwa hiyo Simruhusu mtu yeyote kuukosea ubinadamu Wangu. (Kila kitu Ninachoishi kwa kudhihirisha ni tabia ya uungu—ndiyo maana Nimesema awali, Mimi ni Mungu Mwenyewe aliyeuzidi sana ubinadamu wa kawaida.) Hakika Sitamsamehe yeyote anayenikosea, nami

Nitamsababisha aangamie milele! Kumbuka! Haya ndiyo Nimeamua; kwa maneno mengine, hii ni sehemu muhimu ya amri Zangu za utawala. Kila mtu anapaswa kuona hili: Mtu Niliye ni Mungu, na zaidi ya hayo, Mungu Mwenyewe. Lazima jambo hili liwe wazi sasa! Sizungumzi ovyo ovyo. Mimi husema na kuonyesha kila kitu wazi, mpaka uelewe kabisa.

Hali ni yenye wasiwasi mno; si nyumbani Mwangu tu, lakini hata zaidi nje ya nyumba Yangu, Nawasihi kwamba sharti mlishuhudie jina Langu, muishi kwa kunidhihirisha, na kunishuhudia katika hali zote. Kwa sababu hizi sasa ni nyakati za mwisho, kila kitu kiko tayari sasa na kila kitu kinabaki katika umbo lake la asili, na hakitabadilika kamwe. Wale ambao wanapaswa kutupwa watatupwa, na wale ambao wanapaswa kuhifadhiwa watahifadhiwa. Msijaribu kusimama imara kwa nguvu au kujitenga. Msiuvuruge usimamizi Wangu au kuuharibu mpango Wangu. Kwa watu, daima Ninawapenda na kuwahurumia wanadamu, lakini Kwangu, tabia Yangu inatofautishwa kulingana na hatua za kazi Yangu, kwa sababu Mimi ni Mungu wa vitendo Mwenyewe; Mimi ni Mungu wa pekee Mwenyewe! Mimi ni asiyebadilika na anayebadilika milele. Hili ni jambo ambalo hakuna anayeweza kuelewa. Ni wakati tu Nitakapowaambia na wakati Nitakapowaelezea ndipo mtakapoelewa, mtakapofahamu. Kwa wanangu, Mimi ni mwenye upendo, mwenye huruma, mwenye haki, na mwenye kufundisha nidhamu, bali si mwenye kuhukumu (kwa kusema hivyo Ninamaanisha Siwaangamizi wazaliwa wa kwanza). Kwa wale isipokuwa wana Wangu, Ninabadilika wakati wowote kwa kutegemea enzi zinavyobadilika: mwenye upendo, mwenye huruma, mwenye haki, mwadhimu, mwenye kuhukumu, mwenye hasira, mwenye kulaani, mwenye kuchoma, na hatimaye, mwenye kuiangamiza miili yao. Wale ambao wameangamizwa watatoweka pamoja na roho na nafsi zao. Lakini kwa wale ambao hutoa huduma, roho na nafsi zao pekee zitahifadhiwa (kuhusiana na jinsi ya kutia jambo hili katika vitendo hasa, Nitawaambia baadaye, ili mweze kuelewa). Hata hivyo, hawatakuwa na uhuru kamwe na hawataachiliwa huru kamwe, kwa sababu wako chini ya watu Wangu, na wako chini ya udhibiti wa watu Wangu. Sababu ambayo Niliwachukia watendaji huduma sana ni kwamba wote ni vizazi vya joka kuu jekundu, na wale ambao sio watendaji huduma pia ni vizazi vya joka kuu jekundu. Kwa maneno mengine, wale wote ambao si wazaliwa wa kwanza ni vizazi vya joka kuu jekundu. Ninaposema kwamba wale walio katika hali ya kuteseka milele hunipa sifa za milele, Ninamaanisha kwamba watatoa huduma Kwangu milele. Jambo hili ni la hakika kabisa. Watu hao watakuwa watumwa, ng'ombe, na farasi daima. Ninaweza kuwachinja wakati wowote, na Ninaweza kuwatawala Nipendavyo, kwa sababu wao ni vizazi vya joka kuu jekundu na hawana tabia Yangu. Kwa kuwa wao ni vizazi vya joka kuu jekundu, wana tabia yake, yaani, wana tabia ya wanyama. Hii ni ya kweli kabisa, na isiyobadilika milele! Hii ni kwa sababu haya yote yamejaaliwa na Mimi. Hakuna mtu anayeweza kuyabadilisha hili (Ninamaanisha, Sitamruhusu mtu yeyote kutenda kinyume na sheria hii);

ukijaribu, Nitakuangusha!

Mnapaswa kuona kutoka kwa siri ambazo Mimi hufichua hatua ambayo mpango Wangu wa usimamizi na kazi Yangu vimeendelea hadi kiwango kipi, kuona kile Ninachofanya katika mikono Yangu, kuona wale ambao hukumu Zangu na ghadhabu Yangu huwafika. Hii ni haki Yangu. Kulingana na siri ambazo Nimefichua, Ninapanga kazi Yangu nami Ninausimamia mpango Wangu. Hakuna mtu anayeweza kubadilisha hili—;lazima lifanyike hatua kwa hatua, kufuatana na matamania Yangu. Siri ni njia ya utendaji wa kazi Yangu, nazo ni ishara kwa ajili ya hatua katika mpango Wangu wa usimamizi. Hakuna mtu atakayeongeza au kuondoa chochote kutoka kwa siri Zangu kwa sababu kama siri si sahihi, njia si sahihi. Kwa nini Ninafichua siri Zangu kwenu sasa? Sababu ni nini? Nani kati yenu anaweza kusema waziwazi? Na Nimesema kuwa siri ni njia, kwa hiyo njia hii inamaanisha nini? Ni mchakato ambao mnapitia kutoka katika nyama hadi mwilini, na hii ni hatua muhimu. Baada ya kufichua siri Zangu, dhana za watu zinaondolewa hatua kwa hatua na mawazo yao yanadhoofishwa hatua kwa hatua. Huu ni mchakato wa kuingia katika ulimwengu wa kiroho. Kwa hiyo Ninasema kuwa kazi Yangu hufanyika katika hatua, nayo si ya mashaka—huu ni ukweli, na hii ndiyo njia Yangu ya kufanya kazi. Hakuna mtu anayeweza kubadilisha hili na hakuna mtu anayeweza kufanya hili kwa sababu mimi ni Mungu wa pekee Mwenyewe! Kazi Yangu inakamilishwa na Mimi mwenyewe. Ulimwengu dunia mzima unadhibitiwa na Mimi peke Yangu, na kupangwa na Mimi peke Yangu. Ni nani anayethubutu kutonisikiliza? (Kwa kusema “Mimi peke Yangu” Namaanisha Mungu Mwenyewe, kwa sababu mtu Niliye ni Mungu Mwenyewe, hivyo usishikilie dhana zako mwenyewe kwa nguvu.) Ni nani anayethubutu kunipinga? Ataadhibiwa vikali! Mmeona matokeo ya joka kuu jekundu! Huo ndio mwisho wake, lakini pia ni jambo lisiloepukika. Lazima kazi ifanywe nami binafsi ili liaibishwe, haliwezi hata kuinuka, na litaangamizwa milele yote! Sasa Ninaanza kufichua siri. (Kumbuka! Siri nyingi ambazo zimefichuliwa ni mambo ambayo mara nyingi ninyi husema kwa vinywa vyenu lakini ambayo hakuna mtu anayeelewa.) Nimesema kuwa mambo yote ambayo watu wanaona kama hayajakamilika yameshakamilika machoni Pangu, na mambo ambayo Mimi naona kama ndiyo yanaanza tu huonekana yameshakamilika kwa watu. Je, hii ni kweli kinzani? Sio. Watu wanafikiri hivyo kwa sababu wana fikira na mawazo yao wenyewe. Mambo ambayo Mimi hupanga hukamilika kupitia kwa maneno Yangu (huanzishwa Ninaposema yaanzishwe na hukamilika Ninaposema yakamilike), lakini haionekani Kwangu kuwa mambo ambayo Nimesema yamekamilika. Hii ni kwa sababu kuna ukomo wa muda kwa mambo Ninayoyafanya, kwa hiyo Nayaona mambo hayo kama yasiyokamilika, lakini katika macho ya kimwili ya watu (kwa sababu ya tofauti katika dhana ya wakati) yameshakamilika. Sasa watu wengi wananitilia shaka kwa sababu ya siri Zangu zilizofichuliwa. Kwa sababu ya mwanzo wa ukweli, kwa sababu nia Zangu hazilingani na fikira

za watu, wao ni wenye upinzani kunielekea nao hunikataa. Huyu ni Shetani akijinasa mtegoni katika hila zake mwenyewe. (Wanataka kupokea baraka, lakini hawakufikiri kwamba Mungu hangekubaliana na fikira zao wenyewe kwa kiwango hiki, kwa hivyo wanakimbia.) Hii pia ni athari ya kazi Yangu. Watu wote wanapaswa kunisifu, washangilie kwa ajili Yangu, na wanipe utukufu. Bila shaka kila kitu kiko mikononi Mwangu na kila kitu kiko ndani ya hukumu Yangu. Watu wote wanapotiririka mlimani Kwangu, wazaliwa wa kwanza wanaporudi wakiwa washindi, huo ndio mwisho kwa mpango Wangu wa usimamizi. Ni wakati wa kukamilika kwa miaka Yangu elfu sita ya mpango wa usimamizi. Mimi binafsi Nimepanga yote. Nimeshasema hili mara nyingi. Kwa kuwa bado mnaishi ndani ya mawazo yenu Ninasisitiza hili tena na tena, ili msifanye makosa hapa na kuuharibu mpango Wangu. Watu hawawezi kunisaidia wala hawawezi kushiriki katika usimamizi Wangu, kwa sababu sasa bado ninyi ni wa mwili na damu (ingawa ninyi ni Wangu, bado mnaishi katika mwili). Kwa hiyo Nasema, wale walio wa mwili na damu hawawezi kupokea urithi Wangu. Hii pia ndiyo sababu kuu ya kuwafanya mwingie katika ulimwengu wa kiroho.

Duniani, mitetemeko ya ardhi ni mwanzo wa maafa. Kwanza, Ninaufanya ulimwengu, yaani dunia, ubadilike. Hiyo inafuatwa na mapigo na njaa. Huu ni mpango Wangu, hizi ni hatua Zangu, nami Nitakihamasisha kila kitu kunitumikia, ili kuukamilisha mpango Wangu wa usimamizi. Kwa hiyo ulimwengu dunia wote utaangamizwa, hata bila Mimi kuingilia moja kwa moja. Nilipopata mwili mara ya kwanza na kusulubishwa msalabani, dunia ilitetemeka kwa nguvu sana; itakuwa vivyo hivyo mwishowe. Mitetemeko ya ardhi itaanza wakati huo huo Nitakapoingia katika ulimwengu wa kiroho kutoka katika mwili. Kwa hiyo Nasema, bila shaka wazaliwa wa kwanza hawatapitia maafa. Watu ambao si wazaliwa wa kwanza wataachwa katika maafa na kuteseka. Kwa hiyo, kwa wanadamu, kila mtu yuko tayari kuwa mzaliwa wa kwanza. Katika jakamoyo za watu si kwa ajili ya kufurahia baraka, bali kwa ajili ya kuepuka kupitia maafa. Hii ni hila ya joka kuu jekundu. Lakini Sitaliruhusu litoroke kamwe. Nitalisababisha lipitie adhabu Yangu kali na bado lisimame na kunitolea huduma (hii inamaanisha kuwafanya wana Wangu na watu Wangu kuwa kamili), Niliache lilaghaiwe daima na njama zake lenyewe, likubali hukumu Yangu milele, na likubali uunguzaji Wangu milele. Hii ndiyo maana ya kweli ya kuwafanya watendaji huduma wanisifu (kuwatumia kufichua uwezo Wangu mkubwa). Sitaliruhusu joka kuu jekundu liingie kisirisiri ndani ya ufalme Wangu, na Sitalipa joka kuu jekundu haki ya kunisifu! (Kwa sababu halistahili, halistahili kamwe!) Nitalisababisha tu kutoa huduma Kwangu hadi milele! Nitalisababisha tu linisujudie. (Wale wanaoangamizwa ni bora zaidi kuliko wale walio katika hali ya kuteseka milele. Maangamizi ni adhabu kali ya muda mfupi tu, lakini wale walio katika hali ya kuteseka milele watapitia adhabu kali milele, kwa hiyo Mimi hutumia “kusujudu.” Kwa sababu watu hawa huingia nyumbani Mwangu kisirisiri na

kufurahia neema Yangu nyingi nao wana ufahamu fulani kunihusu, Mimi hutumia adhabu kali. Kwa wale walio nje ya nyumba Yangu, unaweza kusema kuwa wasiojua hawatateseka.) Katika fikira za watu, wanadhani kuwa wale ambao wanaangamizwa ni wabaya zaidi kuliko wale ambao wako katika mateso ya milele, lakini badala yake, wale walio katika hali ya kuteseka milele wanapaswa kuhukumiwa kwa ukali milele, na wale wanaoangamizwa watarudia hali ya kutokuwepo milele.

Sura ya 109

Ninatoa matamko kila siku, kuzungumza kila siku, na kufichua ishara Zangu kuu na shani kila siku. Haya yote ni kazi ya Roho Wangu. Machoni pa watu Mimi ni mwanadamu tu, lakini hasa ni katika mwanadamu huyu ndipo Ninafichua vyote Vyangu na nguvu Yangu kuu.

Kwa kuwa watu humpuza mwanadamu Niliye na huyapuza matendo Yangu, wanafikiri kuwa hivi ni vitu ambavyo hufanywa na wanadamu. Lakini mbona hufikiri: Je, watu wanaweza kutimiza yale Ninayoyatenda? Watu hawanijui kwa kiwango hiki, hawayaelewi maneno Yangu. Wanadamu waovu, waliopotoka! Je, Nitakumeza lini? Je, Nitakuzika katika ziwa la moto wa jehanamu lini? Ni mara nyingi ambapo Nimefukuzwa kutoka katika kundi lenu, mara nyingi watu wamenitukana, kunidhihaki na kuniharibia jina mara ngapi, na ni mara nyingi watu wamenihukumu waziwazi na kuniasi. Wanadamu vipofu! Je, hamjui kuwa ninyi ni konzi la matope mikononi Mwangu tu? Je, hamjui kuwa ninyi ni vitu vya uumbaji Wangu. Sasa, ghadhabu Yangu inaachiliwa na hakuna mtu ambaye anaweza kujikinga dhidi yake. Anaweza tu kuomba huruma tena na tena. Lakini kwa kuwa kazi Yangu imepiga hatua hadi kiwango hiki, hakuna anayeweza kuibadilisha. Wale ambao wameumbwa lazima warudi kwenye matope. Si kwamba Mimi ni mdhalimu, lakini kwamba ninyi ni wapotovu kupita kiasi na wakaidi, na ni kwa sababu mmekamatwa na Shetani na kuwa ala zake. Mimi ndimi Mungu mtakatifu Mwenyewe, Siwezi kuchafuliwa, na Siwezi kumiliki hekalu najisi. Kuanzia sasa kuendelea, ghadhabu Yangu iliyo kali sana (kali zaidi kuliko hasira) itaanza kumwagwa juu ya mataifa na watu wote, na itaanza kuwaadibu watu wote duni sana ambao hutoka Kwangu ila hawanijui Mimi. Ninawachukia wanadamu mno, na Sitakuwa na huruma tena, ila Nitashusha kwa wingi laana Zangu zote. Bila shaka hakutakuwa na huruma wala upendo, kila kitu kitateketezwa mpaka kikose kuwepo, na ufalme Wangu pekee ndio utasalia, ili kwamba watu Wangu watanisifu katika Nyumba Yangu, kunipa utukufu, na kunichangamsha milele (hii ndiyo kazi ya watu Wangu). Mkono Wangu utaanza kuwaadibu rasmi wale walio nje na ndani ya nyumba Yangu. Hakuna mwovu yeyote atakayeweza kuepuka mshiko Wangu na hukumu. Kila mtu lazima apite majaribu haya na kuniabudu Mimi. Huu ni uadhama Wangu, na zaidi ya hayo, ni amri ya utawala ambayo Ninawatangazia waovu. Hakuna mtu anayeweza kumwokoia yeyote mwingine. Wanaweza tu

kuwachunga wao wenyewe, lakini bila kujali wanalofanya, hawataweza kuepuka mkono Wangu wa kuadibu. Sababu ya kuwa imesemekana kwamba amri Zangu za utawala ni kali imefichuliwa hapa. Huu ni ukweli ambao kila mtu anaweza kuuona kwa macho yake.

Ninapoanza kupata hasira, pepo wote, wakubwa na wadogo, watatoroka kwa vurumai, wakiwa na hofu kuu kuwa mkono Wangu utawaua. Lakini hakuna mtu yeyote anayeweza kuepuka kutoka mikononi Mwangu. Mimi hushikilia vifaa vyote vya mateso, mkono Wangu huvithibiti vyote, kila kitu kiko katika mshiko Wangu, na hakuna mtu anayeweza kujikomboa. Hii ni hekima Yangu. Nilipokuja katika eneo la binadamu, Nilikuwa nimekwisha kumaliza aina zote za kazi ya matayarisho, Nikiweka msingi wa kuanzisha kazi Yangu miongoni mwa wanadamu (kwa sababu Mimi ndimi Mungu mwenye hekima, na Mimi hushughulikia kile kinachopasa kufanywa na kile ambacho hakipasi kufanywa vizuri). Baada ya kila kitu kupangwa vizuri, Nilipata mwili na Nikaja katika eneo la mwanadamu, lakini hakuna mtu aliyenitambua. Kando na hao Niliowapa nuru, wana wote wa uasi hunifanyia kiburi, hunifedhehesha, na kunidharau. Lakini mwishowe, Nitawafanya kuwa na adabu na watiifu. Ingawa kwa watu inaonekana kuwa Sifanyi mengi, kazi Yangu kubwa tayari imetamatishwa. (Watu wote humtii kikamilifu mwanadamu Niliye katika neno na moyo. Hii ndiyo ishara.) Leo, Ninainuka na kuadibu aina zote za roho mbaya zinazoniasi. Bila kujali zimenifuata kwa muda gani, lazima ziondoke katika upande Wangu. Simtaki yeyote ambaye ananipinga (ni wale wanaokosa ufahamu wa kiroho, wale ambao wamepagawa na roho mbaya kwa muda, na wale wasionijua). Simtaki hata mmoja wao! Wote wataondolewa, na kuwa wana wa kuangamia kabisa! Baada ya kunifanyia huduma leo, lazima wote waondoke! Msibaki katika nyumba Yangu, msiwe watovu wa nidhamu wala wa kutofanya kazi tu. Wale walio wa Shetani wote ni wana wa ibilisi, na wataangamia milele. Wale wote wanaonikaidi wataondoka upande Wangu kimya, hivyo mwendo wa kazi Yangu utakuwa wa kutozuiwa zaidi bila madakizo zaidi. Vitu vyote vitafanywa kwa amri Yangu, bila vikwazo vyovyote wala mapingamizi yoyote. Vyote vitaanguka machoni Pangu na kuharibiwa katika uteketezaji Wangu. Hili linaonyesha uweza Wangu and hekima Yangu kamili (kile Nilichofanya katika wazaliwa Wangu wa kwanza). Hili litaongeza utukufu mkubwa zaidi kwa jina Langu, na kuongeza utukufu mkuu Kwangu. Kutoka kwa kile Ninachofanya na kutoka kwa toni ya sauti Yangu, ninyi nyote mnaona kuwa Nimemaliza kazi Yangu katika nyumba Yangu kikamilifu na Nimeanza kuyageukia mataifa yasiyo ya Uyahudi. Ninaanza kazi Yangu hapo na kutekeleza hatua inayofuata ya kazi Yangu.

Maneno Yangu mengi hayalingani na dhana zenu, lakini wana Wangu, msiondoke. Kwamba hayalingani na dhana za binadamu haimaanishi kuwa si sauti Yangu. Ni hasa kwa sababu ya hili kwamba inaweza kuthibitishwa kuwa ni sauti Yangu. Kama ingelingana na dhana za binadamu, basi hiyo ingekuwa kazi ya roho mbaya. Hivyo, lazima mtie bidii zaidi katika

maneno Yangu, mfanye Ninayoyafanya, na kupenda Ninachokipenda. Hii enzi ya mwisho pia ni enzi ambapo maafa yote hutokea tena, na hata zaidi enzi ambapo Ninafichua tabia Zangu zote. Mabaragumu Yangu yote matakatiifu yatakapoanza kupigwa, watu kwa kweli wataogopa, na kisha hakuna atakayethubutu kufanya maovu, lakini badala yake watasujudu mbele Yangu, wakitambua vyema hekima Yangu na uweza Wangu. Mimi, hata hivyo, ndimi Mungu Mwenyewe mwenye hekima! Je, ni nani awezaye kunikanusha? Na ni nani anayethubutu kuinuka kunipinga? Ni nani anayethubutu kutokubali hekima Yangu? Je, nani anayethubutu kutojua uweza Wangu? Roho Wangu anapofanya kazi kubwa kila mahali, watu wote hujua uweza Wangu, lakini lengo Langu bado halijafikiwa. Nataka watu waone uweza Wangu kwa sababu ya ghadhabu Yangu, waone hekima Yangu, na waone utukufu wa nafsi Yangu. (Haya yote ni katika wazaliwa wa kwanza, bila makosa yoyote. Kando nao, hakuna anayeweza kuwa sehemu ya nafsi Yangu; hili limeamuriwa na Mimi.) Katika nyumba Yangu, kuna mafumbo yasiyokuwa na mwisho ambayo watu hawawezi kuyaelewa. Ninapozungumza, watu husema kuwa Sina huruma kabisa, wao husema kuwa watu wengi mno tayari hunipenda kwa kiwango fulani, lakini kwa nini Nasema kuwa wao ni wa ukoo wa joka kuu jekundu? Na kwa nini Nitawaacha mmoja baada ya mwingine? Je, si ni vema kuwa na watu wengi zaidi katika nyumba Yangu? Lakini bado Natenda hivi. Hakuwezi kuwa na mmoja zaidi wala mmoja chache kuliko nambari Niliyoamua kabla. (Hii ni amri Yangu ya utawala. Haiwezi tu kutobadilishwa na watu, lakini hata Mimi mwenyewe Siwezi kuibadilisha, kwa kuwa Siwezi kushindwa mbele ya Shetani. Haya yametosha kuonyesha hekima Yangu na uadhama Wangu. Mimi ndimi Mungu mmoja Mwenyewe. Ni ukweli tu kwamba watu huinama mbele Yangu; Sishindwi mbele ya watu.) Hii hasa ndiyo hoja ambayo humuaibisha Shetani zaidi. Watu wote ambao Nimewachagua ni wanyenyekevu, watiifu, ni wasikivu na waaminifu, na wanaweza kunihudumia kwa unyenyekevu na katika mashaka. (Shetani alitaka kutumia hili kunifedhehesha, lakini Nilimpigana.) Tabia Yangu inaweza kuonekana kutoka kwa watu hawa. Wakati ambapo Nimerudi baada ya ushindi vitani, Nitawatia mafuta wazaliwa Wangu wa kwanza ili wawe wafalme katika Ufalme Wangu, na ni wakati huo tu ambapo Nitaanza kupumzika, kwa kuwa wazaliwa Wangu wa kwanza watakuwa wafalme pamoja Nami. Wazaliwa Wangu wa kwanza huniwakilisha Mimi, na hunionyesha Mimi. Katika unyenyekevu wao na huduma yao isiyo wazi, wao hunitii, katika uaminifu wao hutekeleza maneno Yangu, katika uaminifu wao huyasema yale Ninayoyasema, na katika unyenyekevu wao huleta utukufu kwa jina Langu (bila ufidhuli au ukatili, bali kwa uadhama na ghadhabu). Wazaliwa Wangu wa kwanza! Ni wakati wa kuhukumu ulimwengu dunia! Ninawapa baraka, Ninawapa mamlaka, na Ninawatuza baraka! Kila kitu kimekwisha kutimizwa, na vyote vinathibitiwa nanyi, kupangwa nanyi, kwa kuwa Mimi ni Baba yenu, Mimi ndimi mnara wenu ulio dhabiti, Mimi ndimi kimbilio lenu, Mimi ndimi usaidizi wenu, na hata zaidi Mimi ndimi Yule mwenye Uweza wako,

na Mimi ni kila kitu chako! Kila kitu kiko mikononi Mwangu, na kila kitu pia kiko mikononi mwenu. Si leo tu, lakini pia jana, na hata kesho! Je, hii haifai kuadhimishwa? Je, haifai shangwe yenu? Ninyi nyote, kubalini fungu mnalostahili kutoka Kwangu. Ninakupa kila kitu changu, na Sihifadhi hata kipande kimoja, kwa sababu mali Yangu yote ni yenu, na utajiri Wangu uko juu yenu. Hii ndiyo sababu Nilisema “vyema sana” baada ya kuwaumba.

Je, mnajua yule anayeelekeza kile mnachofanya, kufikiria, na kusema leo? Na kila kitu mnachofanya ni cha nini? Ninawauliza, mnahudhuria vipi karamu ya ndoa ya Mwanakondoo? Je, ni leo? Ama ni wakati ujao? Je, karamu ya ndoa ya Mwanakondoo ni nini? Hamjui, siyo? Basi Ninawaelezea: Nilipokuja katika eneo la binadamu, Nilikuwa nimeandaa aina zote za watu, mambo, na vitu ili kuhudumia mtu Niliye leo. Sasa kwa kuwa kila kitu kimekamiliika, Ninawatupa pembeni watendaji huduma. Je, hili linahusiana vipi na karamu ya ndoa? Watu hawa wanaponihudumia, yaani, Ninapofanywa kuwa Mwanakondoo, Ninaonja ladha ya karamu ya ndoa. Hivyo ni kusema kuwa, uchungu wote Nilioupitia, vitu vyote ambavyo Nimefanya, vitu vyote ambavyo Nimesema, kila mtu Niliyepatana naye, na kila ambacho Nimekifanya katika maisha Yangu vimejumuisha karamu ya ndoa. Baada ya mwanadamu Niliye kupakwa mafuta, mlinifuata (wakati huu Nilikuwa Mwanakondoo), hivyo chini ya uongozi Wangu, mmezipitia aina zote za uchungu, maafa, kuachwa na kutukanwa na dunia, kuachwa na familia, na mnaishi katika baraka Zangu. Haya yote ni karamu ya ndoa ya Mwanakondoo. Mimi hutumia “karamu ya ndoa” kwa sababu yote Niliyowaelekeza katika kufanya ni kwa ajili ya kuwapata. Lakini haya yote ni sehemu ya karamu. Katika siku zijazo, mtu aweza pia kusema leo, kila kitu mnachofurahia, kila kitu mnachopata, na nguvu ya kifalme mnayoshiriki pamoja nami, yote ni karamu. Upendo Wangu huja kwa wale wote wanaonipenda. Wale Ninaowapenda watasalia hadi milele, hawataondolewa asilani, watakuwa katika upendo Wangu daima. Ni milele!

Sura ya 110

Kila kitu kitakapofichuliwa utakuwa wakati ambapo Nitapumzika, na hata zaidi, utakuwa wakati ambapo kila kitu kitakuwa sawa. Mimi hufanya kazi Yangu binafsi; Mimi hupanga kila kitu na kusafidi kila kitu Mwenyewe. Nitakapotoka Sayuni na Nitakaporejea, wazaliwa Wangu wa kwanza watakapokuwa wamekamilishwa na Mimi, Nitakuwa Nimemaliza kazi Yangu kubwa. Katika mawazo ya watu kitu ambacho kinafanywa ni sharti kiweze kuonekana na kuguswa, lakini jinsi Ninavyoona, kila kitu ni kikamilifu wakati ambapo Ninafanya mpango Wangu. Sayuni ndipo Ninapoishi na ndiyo hatima Yangu; ni hapo ambapo Mimi hufichua uweza Wangu, na ni hapo ndipo wazaliwa Wangu wa kwanza pamoja Nami tutashiriki furaha zetu za familia. Ni hapo ndipo Mimi nitaishi nao milele yote. Sayuni, mahali pazuri; Sayuni, mahali ambapo watu hutamani sana; watu wasiohesabika wamepatamani katika enzi zote, lakini kutoka

mwanzo, hakuna mtu hata mmoja ambaye ameingia Sayuni. (Wala hata watakatifu na manabii wowote tangu enzi zilizopita. Hii ni kwa sababu Nawachagua wazaliwa Wangu wa kwanza katika siku za mwisho; na wote wanazaliwa wakati huu; na kupitia hii rehema Yangu na neema Yangu ambayo Nimezungumzia ni dhahiri zaidi.) Kila mtu ambaye sasa ni mzaliwa Wangu wa kwanza ataingia Sayuni pamoja na Mimi na kufurahia baraka hiyo. Mimi nawainua wazaliwa Wangu wa kwanza hadi kiwango fulani kwa sababu wana uhodari Wangu na mfano Wangu wenye utukufu na wana uwezo wa kuwa na ushuhuda Wangu na pia kunitukuza na kuishi kwa kunidhihirisha. Hata zaidi, wana uwezo wa kumshinda Shetani na kuliaibisha joka kubwa jekundu. Na ni kwa sababu wazaliwa Wangu wa kwanza ni mabikira safi; wao ni kile Ninachokipenda, na ni wale ambao Nimewachagua na kupendelea. Sababu ya Mimi kuwainua wao ni kuwa wana uwezo wa kusimama katika nafasi zao wenyewe na wana uwezo wa kunitumikia kwa unyenyekevu na kimya na kuwa na ushuhuda Wangu mkubwa Nimetumia nguvu Yangu yote kwa wazaliwa Wangu wa kwanza na kwa makini Nimepanga watu, matukio, na mambo ya aina zote kwa ajili ya huduma zao. Mwishowe Mimi nitamfanya kila mtu aone utukufu Wangu mzima kutoka kwa wazaliwa Wangu wa kwanza, na Nitamfanya kila mtu aridhike kabisa na Mimi kwa sababu ya wazaliwa Wangu wa kwanza. Sitamlazimisha pepo yeyote, na Sina hofu nao kukimbia kote au kutojali kwao kwa sababu Ninao washahidi, na Nina mamlaka mikononi Mwangu. Sikilizeni, watu wa aina ya Shetani! Makusudi ya kila neno ambalo Ninalitamka na kila kitu ambacho Ninafanya ni ili kuwakamilisha wazaliwa Wangu wa kwanza. Kwa hivyo ni lazima wewe usikilize kwa makini amri Zangu na kutii Wazaliwa Wangu wa kwanza; vinginevyo Nitakushughulikia kwa kukufanya upitie maangamizo ya mara moja! Wazaliwa Wangu wa kwanza tayari wameanza kutekeleza amri Zangu za utawala kwa sababu ni wao tu wanaostahili kushikilia kwa nguvu kiti Changu cha enzi, na tayari Nimewapaka mafuta. Yeyote ambaye hatii wazaliwa Wangu wa kwanza kwa hakika hana manufaa. Bila shaka ametumwa na joka kubwa jekundu kuvuruga mpango Wangu wa usimamizi, na mwovu wa aina hiyo atasukumwa nje ya nyumba Yangu mara moja. Sitaki kitu cha aina hiyo kinifanyie huduma—kitakumbana na uharibifu wa milele, na kitakumbana nao haraka sana, bila kuchelewa! Wale ambao hunihudumia ni lazima tayari wamepokea idhini Yangu; lazima wawe watiifu na wasitilie maanani gharama wanayolipa. Kama ni waasi hawastahili kutoa huduma Kwangu na Sihitaji kiumbe kama huyo. Watakimbia kwa haraka—Mimi siwataki kabisa! Lazima uwe na hakika kuhusu hili sasa! Wale ambao hufanya huduma kwa ajili Yangu ni lazima waifanye vizuri na wasisababisha matatizo. Ukihisi kuwa huna matumaini na uanze kusababisha matatizo—Nitakumaliza mara moja. Je, ninyi ambao mnatoa huduma kwa ajili Yangu mna uhakika kuhusu hilo? Hii ni amri Yangu ya utawala.

Kuwa na ushuhuda Wangu ni jukumu la wazaliwa Wangu wa kwanza, hivyo Siwahitaji

ninyi kwamba mfanye lolote kwa ajili Yangu—Nitaridhishwa mradi tu mtekeleze wajibu wenu vizuri na kufurahia baraka ambazo Nimewapa. Niliposafiri katika ulimwengu mzima na miisho ya dunia, Niliwachagua na kuwafanya wazaliwa Wangu wa kwanza wawe wakamilifu. Hili ni jambo ambalo Nilikamilisha kabla ya Mimi kuumba ulimwengu; hakuna mtu kati ya wanadamu analijua hilo, lakini kazi Yangu ilitimizika kwa utulivu. Hilo halikubaliani na fikira za binadamu! Lakini ukweli ni ukweli na hakuna anayeweza kuubadilisha. Maepo wakubwa kwa wadogo wamefichua umbo lao la kweli kutoka kwa unafiki wao, na wamekuwa chini ya adhabu Yangu kwa viwango tofauti. Kuna hatua katika kazi Yangu na kuna hekima katika maneno Yangu. Je, mmeona kitu chochote kutoka kwa kile Ninachosema na kufanya? Je, ni kufanya tu vitu na kusema mambo? Je, maneno Yangu ni makali, au ya kuhukumu, au ya kufariji tu? Hiyo ni rahisi sana, lakini kwa watu, kuona hiyo si rahisi hata kidogo. Hakuna hekima, hukumu, haki, uadhama, na faraja pekee katika maneno Yangu, lakini hata zaidi lina kile Nilicho nacho na kile Nilicho. Kila mojawapo ya maneno Yangu ni mafumbo ambayo hayawezi kufichuliwa na watu. Maneno Yangu hayaeleweki kabisa, na ingawa mafumbo yamefichuliwa, kulingana na uwezo wa wanadamu bado ni nje ya wigo wao wa mawazo na ufahamu. Neno rahisi sana Kwangu kuelewa ni jambo gumu zaidi kwa watu kuelewa, kwa hivyo tofauti kati ya Mimi na mwanadamu ni tofauti kati ya mbingu na nchi. Hii ndiyo sababu Nataka kubadilisha kabisa umbo la wazaliwa Wangu wa kwanza na kuwafanya wao kuingia katika mwili kabisa. Katika siku zijazo, hawataingia tu katika mwili kutoka kwa nyama, lakini watabadilisha umbo lao ndani ya mwili kwa viwango tofauti. Huu ni mpango Wangu. Hili ni jambo ambalo wanadamu hawawezi kulifanya—wao hawana namna ya kufanya hivyo kabisa—hivyo sasa hata kama Ningewaambia kwa kina, bado msingeelewa. Unaweza tu kuingia katika hali isiyo ya kawaida. Hii ni kwa sababu Mimi ni Mungu Mwenyewe mwenye busara.

Mnapoona mafumbo nyote mna mjibizo kiasi. Hata ingawa hamkubali au kukiri hayo katika nyoyo zenu, mnayakiri kwa maneno yenu. Mtu wa aina hii ni yule mdanganyifu zaidi, na Ninapofichua mafumbo, Nitawaondoa na kuwaacha mmoja baada ya mwingine. Lakini kila kitu Nifanyacho ni kwa hatua. Sitendi mambo kwa haraka au kufikia hitimisho bila kufikiri; hii ni kwa sababu Nina tabia ya uungu. Watu hawawezi kabisa kuona bayana Ninachofanya sasa, Nitakachofanya katika hatua Yangu ifuatayo. Nitakaponena tu kuhusu mbinu Yangu ya kufanya kazi katika hatua ifuatayo ndipo watu wataweza kunifuata na kupiga hatua moja mbele. Kila kitu hufanyika ndani ya maneno Yangu, kila kitu hufichuliwa ndani ya maneno Yangu, hivyo hakuna yeyote anayetakiwa kuwa na pupa—kutoa huduma Kwangu vizuri kunatosha. Kabla ya enzi Nilifanya utabiri kuhusu mtini, lakini katika enzi zote hakuna yeyote aliyekuwa ameuona mtini na hakuna yeyote ambaye angeweza kuuelezea, na hata ingawa maneno haya yalitajwa katika sifa za awali, hakuna aliyejua maana yake ya kweli. Maneno haya yaliwachanganya watu kama

tu “janga kubwa,” na lilikuwa fumbo ambalo kamwe Sikutandua kwa wanadamu. Watu walidhani kuwa mti wa tini labda ulikuwa aina ya mti mzuri wa matunda, au labda kuwa zaidi ya hayo uliashiria watakatifu, lakini bado walikuwa mbali sana na maana halisi. Nitawaambia hili wakati ambapo Nitafungua kitabu Changu katika siku za mwisho. (Kitabu kinahusu maneno yote ambayo Nimeyanena, maneno Yangu katika siku za mwisho—haya yote yako ndani yake.) Mti wa tini unahusu amri Zangu za utawala, na kila mojawapo ya amri Zangu za utawala, lakini hii ni sehemu moja tu ya hayo. Kuchipua kwa mtini kunahusu Mimi kuanza kufanya kazi na kuzungumza katika mwili, lakini amri Zangu za utawala hazikuwa zimetambulishwa bado (ndio sababu hilo lilikuwa kabla ya kushuhudiwa kwa jina Langu na hakuna yeyote aliyejua amri Zangu za utawala). Wakati ambapo jina Langu linashuhudiwa na kuenea, wakati ambapo linasifiwa na watu wote, wakati ambapo amri Zangu za utawala kuzaa matunda, huo ndio wakati wa mti wa tini kuzaa matunda. Haya ni maelezo kamili na hakuna kitu kilichoachwa—vyote vinafichuliwa (Nasema hivi kwa sababu katika maneno Yangu ya awali, kulikuwa na sehemu ambayo bado Sikuwa Nimefichua kikamilifu; kwa hivyo mlihitajika kusubiri na kutafuta kwa uvumilivu.)

Nitakapowafanya wazaliwa Wangu wa kwanza kamili, Nitafichua utukufu Wangu kamili, kuonekana Kwangu kamili kwa ulimwengu dunia katika mwili, na juu ya watu wote, kwa nafsi Yangu mwenyewe; itakuwa katika Mlima Wangu wa Sayuni, katika utukufu Wangu, na itakuwa hasa katikati ya makelele ya sifa, na maadui Zangu watarudi nyuma kandokando Yangu, wakiteremka katika shimo la kuzimu, ziwa la moto wa jahanamu. Kile ambacho watu wanaweza kuwaza leo kina mpaka na hakilingani na nia Yangu ya asili; hii ndiyo sababu Mimi hulenga dhana na fikira za watu kila siku Ninaponena. Kutakuwa na siku (siku ya kuingia katika mwili), ambapo kile Ninachosema kitakuwa cha kuwafaa kabisa na hakutakuwa na upinzani wowote kabisa, na wakati huo ninyi hamtakuwa tena na mawazo yenu, na baada ya hapo Sitazungumza tena. Kwa kuwa hamna mawazo yenu wenyewe tena, Mimi nitawapa nuru moja kwa moja tu—hii ni baraka inayofurahiwa na wazaliwa Wangu wa kwanza, na huo utakuwa wakati ambapo watatawala pamoja na Mimi kama wafalme. Wanadamu hawaamini katika mambo ambayo hawawezi kufikiria, na hata kama kuna baadhi ya watu ambao wanaamini hayo, ni kwa sababu hasa ya kupatiwa nuru na Mimi. Vinginevyo hakuna yeyote ambaye angeamini, na hili ni jambo ambalo lazima lipitiwe. (Bila kupitia hatua hii, nguvu Yangu kubwa haingeweza kufichuliwa kupitia hiyo, ambayo ina maana kwamba Mimi huyatumia maneno Yangu kuwaondolea watu fikira zao. Hakuna yeyote mwingine anayeweza kufanya kazi hii, na hakuna yeyote anayeweza kuchukua nafasi Yangu. Mimi tu ndimi Ninayeweza kuimaliza, hata hivyo, hiyo si kamili. Lazima Nifanye kazi hii kupitia kwa wanadamu.) Watu hujihisi kuchangamshwa baada ya kusikia maneno Yangu, lakini mwishowe wao wote wanarudi nyuma. Hawana budi ila kufanya

hivyo. Wakati huo huo, kuna mafumbo ambayo watu hawawezi kuyafahamu. Hakuna yeyote anayeweza kufikiria kile ambacho kitatokea na Nitawawezesha kuona hili katika kile ambacho Ninafichua. Kwa njia hiyo mnaweza kuona maana halisi ya msemu Wangu: “Nitang’oa wale wote ambao hawafai kwa ajili ya matumizi Yangu.” Wazaliwa Wangu wa kwanza wana maonyesho mbalimbali na vilevile maadui Wangu. Wote watafichuliwa kwenu, mmoja mmoja. Kumbuka! Yeyote isipokuwa wazaliwa Wangu wa kwanza ana kazi ya pepo wabaya. Wote hao ni vikaragosi wa Shetani. (Hivi punde watafichuliwa mmoja baada ya mwingine, lakini kuna baadhi ambao wanahitaji kufanya huduma hadi mwisho, na baadhi ambao wanahitaji kufanya huduma kwa kipindi cha muda.) Chini ya kazi ya maneno Yangu, wote wataonyesha hali zao za kweli.

Kila taifa, kila mahali, na kila dhehebu kinafurahia ukwasi wa jina Langu. Kwa sababu sasa hivi janga linajiandaa, na liko katika mshiko Wangu, na Ninajiandaa kulimuaga polepole, kila mtu anatafuta njia ya kweli kwa haraka, ambayo ni lazima itafutwe hata kama inamaanisha kulipa gharama nzima. Katika mambo yote Nina muda Wangu mwenyewe. Wakati wowote Ninaposema itakamilishwa, itakamilishwa wakati huo, kwa dakika, kwa sekunde. Hamna yeyote anayeweza kuizuia au kuisimamisha. Hata hivyo, joka kubwa jekundu ni adui Yangu aliyeshindwa. Linatenda huduma kwa ajili Yangu, na linafanya chochote Ninacholiambia bila upinzani wowote. Kweli ni mnyama Wangu wa mzigo. Wakati ambapo kazi Yangu imekamilika, Nitalitupa katika shimo la kuzimu, ndani ya ziwa la moto wa jahanamu (ambayo inarejelea wale ambao wanaangamizwa). Watakaoangamizwa hawataonja kifo tu, lakini wataadhibiwa vikali kwa ajili ya mateso yao Kwangu. Hii ni kazi ambayo bado Nitafanya kupitia watendaji huduma—Nitamfanya Shetani ajichinje mwenyewe na kujiangamiza, kuondoa kabisa ukoo wa joka kubwa jekundu. Hii ni sehemu moja ya kazi Yangu, na baada ya hapo, Nitayageukia mataifa yasiyo ya Uyahudi. Hizi ndizo hatua za kazi Yangu.

Sura ya 111

Mataifa yote zyatabarikiwa kwa sababu Yako; watu wote watanikaribisha kwa shangwe na kunisifu kwa sababu Yako. Ufalme Wangu utafanikiwa na kukua, na utabaki milele. Hakuna mtu ataruhusiwa kuukanyaga na hakuna kitu kitaruhusiwa kuwepo ambacho hakikubaliani na Mimi, kwa sababu Mimi ni Mungu mwenye uadhama na asiyekosewa Mwenyewe. Sikubali mtu yeyote anihukumu na Sikubali mtu yeyote kutolingana na Mimi. Hili linatosha kuonyesha tabia Yangu na uadhama Wangu. Mtu yeyote anaponipinga, Nitamwadhibu kwa wakati Wangu mwenyewe. Kwa nini hakuna mtu ambaye ameniona Nikimwadhibu mtu yeyote? Ni kwa sababu tu wakati Wangu haujafika bado na mkono Wangu bado haujatenda kweli. Ingawa maafa makubwa yametolewa kwa kishindo, hili linazungumzia tu kile ambacho maafa makubwa yanajumuisha,

wakati uhalisi wa maafa makubwa haujamfikia hata mtu mmoja. Je, mmeelewa chochote hata kidogo kutoka kwa maneno Yangu? Nitaanza kuachilia uhalisi wa maafa makubwa leo. Baada ya hili, yeyote atakayenipinga atapigwa chini na mkono Wangu. Zamani Nimewafichua tu watu fulani, na hakuna maafa yoyote makubwa yamefika. Leo ni tofauti na zamani. Kwa kuwa Nimewaambia nyote kuhusu kile kinachojumuisha maafa makubwa, kwa wakati uliopangwa Nitatangaza kwa umma uhalisi wa maafa makubwa. Kabla ya hili, hakuna mtu ambaye ameguswa na maafa makubwa, kwa hivyo watu wengi (yaani, wana wa joka kubwa jekundu) wameendelea kutenda kwa kutojali na kiholela. Wakati ambapo uhalisi unafika vitu hivi vitaridhishwa kabisa. Vinginevyo kila mtu atakuwa na shaka kunihusu, na hakuna mtu atakayekuwa wazi kunihusu. Hii ni amri Yangu ya utawala. Kutoka kwa hili inaweza kuonekana kwamba njia Yangu ya kufanya kazi (ikirejelea njia Yangu ya kufanya kazi katika watu wote) imeanza kubadilika: Katika uzao wa joka kubwa jekundu Ninaonyesha ghadhabu Yangu, Ninaonyesha hukumu Yangu na laana Yangu, na mkono Wangu umeanza kuwadibu wote wanaonipinga. Kwa wazaliwa wa kwanza Ninaonyesha rehema Yangu na upendo Wangu. Hata zaidi katika wazaliwa wa kwanza Ninaonyesha tabia Yangu takatifu na isiyokosewa, Ninaonyesha mamlaka Yangu, na Ninaonyesha nafsi Yangu. Watendaji huduma wametulia kunitolea huduma, na wazaliwa Wangu wa kwanza wanatambulishwa zaidi na zaidi. Kwa kuwapiga chini wale wanaonipinga Ninawaacha watendaji huduma kuona mkono Wangu usiojizuia ili waweze kunitolea huduma kwa hofu na kutetemeka, na Ninawaacha wazaliwa Wangu wa kwanza waone mamlaka Yangu na kunielewa bora zaidi ili waweze kukua katika maisha. Maneno Niliyoyasema katika kipindi cha mwisho (yakiwemo amri za utawala, unabii, na hukumu ya kila aina za watu) yanaanza kutimizwa kwa kufuatana, yaani, watu wataona maneno Yangu yakifanikishwa mbele ya macho yao, waone kwamba hakuna neno lolote Langu ni bure; yote ni ya utendaji. Kabla ya maneno Yangu kutimizwa watu wengi wataondoka kwa sababu hayajatumizwa. Hivi ndivyo Ninavyofanya kazi—si kazi ya fimbo Yangu ya chuma pekee, lakini hata zaidi ni hekima ya maneno Yangu. Kutoka kwa haya, mtu anaweza kuona kudura Yangu na kuona chuki Yangu kwa joka kubwa jekundu. (Hili linaweza kuonekana tu baada ya Mimi kuanza kazi Yangu. Sasa watu wengine wanafichuliwa—ni sehemu ndogo tu ya kuadibu Kwangu, lakini haiwezi kujumuishwa katika maafa makuu. Hili si gumu kuelewa. Hivyo inaweza kuonekana kwamba kuanzia sasa kuendelea njia Yangu ya kufanya kazi itakuwa ngumu hata zaidi kwa watu kuelewa. Leo Nawaambia ili msiwe wadhaifu kwa sababu ya hili wakati utakapofika. Hili ndilo Ninalowaaminia kwa sababu mambo yatafanyika ambayo watu hawajayaona tangu nyakati za zamani, na hilo litafanya kuwa kugumu kwa watu kuweka kando hisia zao na kujidai kwao.) Sababu ya Mimi kutumia mbinu tofauti kuliadhibu joka kubwa ni kwa sababu ni adui Yangu na ni mshindani Wangu. Ni lazima Niangamize uzao wake yote—ni hapo tu ndipo Ninaweza kuondoa chuki kutoka kwa moyo Wangu, na ni hapo tu ndipo Naweza

kuliaibisha joka kubwa jekundu vizuri. Huku tu ndiko kuangamiza joka kubwa jekundu kabisa na kulitupa katika ziwa la moto na kibiriti na shimo lisilo na mwisho.

Sio tu jana, lakini leo pia, na muhimu zaidi, kesho, Nitawaruhusu wazaliwa Wangu wa kwanza kutawala na Mimi na kuungana na Mimi katika kuongoza mataifa yote na katika kufurahia baraka. Nimekamilisha kazi Yangu kwa ufanisi—Nimekuwa nikisema hivyo muda huu wote, na pia inaweza kusemwa kwamba Nilianza kusema hivyo tangu mwanzo wa uumbaji, lakini binadamu hawaelewi kile Ninachokisema. Tangu uumbaji hadi sasa Sijafanya kazi Mimi binafsi; kwa maneno mengine, Roho Wangu hajawahi kumshukia mwanadamu kikamilifu kusema na kufanya kazi. Lakini leo ni tofauti kuliko zamani: Roho Wangu anafanya kazi Yeye binafsi kila mahali katika ulimwengu dunia. Kwa sababu katika siku za mwisho Ninataka kupata kundi la watu watakaotawala mamlakani na Mimi. Kwanza Ninampata mtu ambaye analingana na Mimi, ili aweze kufikiria mzigo Wangu, na baadaye Roho Wangu atamshukia Yeye kabisa kuonyesha sauti Yangu na kuachilia amri Zangu za utawala na kufichua siri Zangu kwa ulimwengu dunia. Roho Wangu atamkamilisha binafsi; Roho Wangu atamfundisha nidhamu binafsi. Kwa sababu Anaishi katika ubinadamu wa kawaida, hakuna mtu anayeweza kuona kwa wazi. Wakati ambapo wazaliwa Wangu wa kwanza wanaingia katika mwili utakuwa wazi kabisa iwapo kile Ninachokifanya sasa ni uhalisi. Bila shaka, machoni pa binadamu, katika dhana ya binadamu, hakuna mtu anayeamini na hakuna mtu anayeweza kuwa mtiifu. Lakini huu ndio uvumilivu Wangu kwa watu. Kwa sababu uhalisi haujakuja bado, kwa hivyo watu hawawezi kuamini na hawawezi kuelewa. Hakujawahi kuwa na yeyote ambaye angeamini maneno Yangu katika dhana zake za binadamu. Watu wote wako namna hii: Wanaamini tu kile ambacho nafsi Yangu ya mwili inasema, au waamini tu sauti ya Roho Wangu. Hili ndilo jambo gumu zaidi kulishughulikia katika watu. Kama hawajaona kitu kikifanyika na macho yao wenyewe, hakuna mtu anaweza kuachilia dhana zake mwenyewe, na hakuna mtu anayeweza kuamini kile Ninachokisema, kwa hivyo Natumia amri Zangu za utawala kuwaadhibu wale wana wa kutotii.

Nimesema mambo kama haya awali: Mimi ndiye wa Kwanza na wa Mwisho, na pia Mimi nasimamia kila kitu kutoka mwanzo hadi mwisho. Katika siku za mwisho, Nitawapata wana washindi wa kiume 144,000. Mnaelewa kiasi kuhusu haya maneno “wana washindi wa kiume”, lakini hamko wazi kuhusu 144,000. Katika dhana za binadamu nambari lazima irejeele idadi ya watu au idadi ya vitu. Kuhusiana na “144,000” kuwabadilisha “wana washindi wa kiume”—“wana 144,000 washindi wa kiume”—watu wanafikiri kwamba kuna wana washindi wa kiume 144,000. Na aidha watu wengine wanafikiri ni maelezo ya kabla na wanaeleza hiyo 140,000 na 4,000 kando. Lakini haya maelezo mawili si sahihi. Hairejelei nambari halisi, na hata zaidi, hairejelei maelezo ya kabla. Kwa binadamu, hakuna mtu ambaye anaweza kupenya hili—watu wote wa vizazi vilivyopita walifikiri inaweza kuwa maelezo ya kabla. Mia moja na arubaini na

nne elfu inashirikishwa na wana washindi wa kiume. Kwa hivyo, 144,000 inarejelea kundi la watu katika siku za mwisho ambao watatawala, na ambao Ninawapenda. Yaani, 144,000 inatafsiriwa kuwa kundi la watu waliotoka Sayuni na ambao watarudi Sayuni. Maelezo kamili ya wana washindi wa kiume 144,000 ni kama yafuatayo: Wao ndio watu waliotoka Sayuni kuja kwa dunia na walipotoshwa na Shetani, na ambao hatimaye watapatwa na Mimi na watarudi Sayuni na Mimi. Kutoka kwa maneno Yangu mtu anaweza kuona hatua za kazi Yangu, kumaanisha kwamba si kitu cha mbali sana kwamba ninyi mtaingia katika mwili. Kwa hivyo Nimeeleza kwa kurudia na kuwakumbusha kuhusu hili. Mtaona kwa wazi, na kutoka kwa maneno Yangu mtatambua njia ya kutenda; kutoka kwa maneno Yangu mtatambua hatua ya kazi Yangu. Ili kutambua hatua ya kazi ya Roho Mtakatifu, ni lazima muimaizi kutoka kwa siri Ninazofichua (kwa sababu hakuna mtu anayeweza kuona na hakuna mtu anayeweza kupenya kazi ya Roho Mtakatifu). Hiyo ndiyo maana Nafichua siri katika siku za mwisho.

Nyumbani Kwangu hakutakuwa na kitu kisichopatana na Mimi, na kutoka sasa kuendelea Nitaanza kusafisha na kutakasa, kidogo kidogo. Miongoni mwa watu, hakuna mtu anayeweza kuingilia kati, na hakuna mtu anayeweza kufanya kazi hii. Hii inafichua kwa nini Nafanya kazi mwenyewe katika siku za mwisho. Na hii ndiyo maana Nimewaambia mara nyingi kwamba mnahitaji tu kufurahia wenyewe na hamhitaji kufanya juhudi yoyote. Ni kupitia hili ambapo nguvu Yangu inafichuliwa, haki Yangu na uadhama vinafichuliwa, na siri Zangu zote ambazo watu hawawezi kuzifungua zinafichuliwa. (Kwa sababu watu hawajawahi kuwa na maarifa yoyote ya mpango Wangu wa usimamizi au ufahamu wowote wa hatua za kazi Yangu, zinaitwa “siri”.) Kile Nitakachopata na kile Nitakachofanya katika siku za mwisho ni siri. Kabla ya wakati Nilipoiumba dunia, Sikuwahi kufanya kile Ninachokifanya leo na Sikuwahi kuwaonyesha watu uso Wangu wa utukufu au sehemu yoyote ya nafsi Yangu; Roho Wangu tu ndiye amefanya kazi kwa watu wengine. (Kwa sababu, tangu wakati wa uumbaji, hakuna mtu ameweza kunidhihirisha na hakuna mtu ameweza kunionyesha, Sijawahi kuwaruhusu watu kuona nafsi Yangu, na Roho Wangu amefanya kazi kwawatu wengine.) Ni leo tu ndiyo Nimefichua sura Yangu ya utukufu na nafsi Yangu kwa watu, na ni sasa tu ambapo wameyaona. Lakini kile mnachoona leo bado hakijakamilika, na bado si kile Ninachowataka muone. Kile Ninachowataka muone kiko katika mwili tu, na sasa hivi bado hakuna mtu anayefikia sharti hili. Katika maneno mengine, hakuna mtu anayeweza kuona nafsi Yangu kabla ya yeye kuingia katika mwili. Kwa hivyo Nasema kwamba Nitaifichua nafsi Yangu kwa ulimwengu dunia Mlimani Sayuni. Kutoka kwa hili inaweza kuonekana kwamba kuingia katika Mlima Sayuni ndiyo sehemu ya mwisho ya mradi Wangu. Wakati wa kuingia katika Mlima Sayuni, ufalme Wangu utakuwa umejengwa kwa ufanisi. Kwa maneno mengine, nafsi Yangu ndiyo ufalme. Wakati ambapo wazaliwa wa kwanza wanaingia katika mwili ni hasa wakati ambapo ufalme utafanyika, kwa hivyo Nimesema kwa

kurudia kuhusu suala la wazaliwa wa kwanza kuingia katika Mlima Sayuni. Hii ndiyo sehemu kuu ya mpango Wangu wote wa usimamizi, ambao hakuna mtu amewahi kuelewa awali.

Punde Ninapobadili njia Yangu ya kufanya kazi kutakuwa na hata vitu zaidi ambavyo vinazidi fikira za binadamu, kwa hivyo kuwa makini kuhusu jambo hili. Kuna vitu ambavyo vinazidi fikira za binadamu, lakini hili halimaanishi kwamba kile Ninachokisema si sahihi. Ni kwamba tu ni muhimu hata zaidi kwa watu kuteseka, na ni muhimu hata zaidi kushirikiana na Mimi. Usiwe asiyezuiwa kwa utukutu au kufuata tu dhana zako mwenyewe. Kwa kuwa wengi wa wale wanaonitolea huduma wanaanguka katika jambo hili. Natumia maneno Yangu kufichua asili ya binadamu na kufichua dhana za binadamu. (Lakini wale wanaonitolea huduma, kwa sababu Sijabadili dhana zao, wanaanguka tu, ilhali Nimebadili dhana za wale walio wazaliwa Wangu wa kwanza na Nimeondoa fikira zao kupitia hili.) Kwa hivyo mwishowe, wazaliwa Wangu wa kwanza wote watakamilishwa kwa sababu ya siri ambazo Nimefichua.

Sura ya 112

Kwamba “maneno na uhalisi huendelea kwa pamoja” ni sehemu ya tabia Yangu ya haki na, kutoka kwa maneno haya, bila shaka Nitamwacha kila mtu aone tabia Yangu yote. Watu hufikiri hili haliwezi kutimizwa, lakini Kwangu ni rahisi na linafurahisha, na halitumii juhudi yoyote. Wakati ambapo maneno Yangu yanatoka mara moja kuna uhalisi ambao kila mtu anaweza kuuona. Hii ndiyo tabia Yangu. Kwa kuwa Nasema kitu kinakamilishwa kwa lazima, vinginevyo Singezungumza. Katika dhana ya binadamu neno “wokovu” linasemwa kwa ajili ya watu wote, lakini hili halilingani na nia Zangu. Zamani Nilisema “Daima Mimi huwaokoa wale ambao ni wajinga na ambao wanatafuta kwa ari” ambapo neno “okoa” lilisemwa kuhusu wale wanaonitolea huduma, na lilimaanisha kwamba Ningewatendea kwa upekee watendaji huduma kama hawa. Kwa maneno mengine, Ningepunguza adhabu kwa watu hao. Hata hivyo, hawa watendaji huduma wasio waaminifu na walio wadanganyifu wangukuwa miongoni mwa walengwa wa uangamizaji, yaani, Ningewapa adhabu kali. (Ingawa wao ni miongoni mwa walengwa wa uangamizaji, ni tofauti sana kuliko wale wanaoangamizwa: Watapokea adhabu kali ya milele, na adhabu ambayo watu hao watapokea ni adhabu ya ibilisi, Shetani. Hii pia ndiyo maana ya kweli ya kile Nilichosema, kwamba watu wale ni uzao wa joka kubwa jekundu.) Lakini Situmii maneno ya aina hizi kuhusu wazaliwa Wangu wa kwanza; badala yake Nasema kwamba Nitawapata tena wazaliwa Wangu wa kwanza na watarudi Sayuni. Kwa hivyo Nimesema daima kwamba wazaliwa Wangu wa kwanza ni waliojaaliwa na waliochaguliwa Wangu. Wazaliwa Wangu wa kwanza walikuwa Wangu mwanzoni, walitoka Kwangu, kwa hivyo lazima warudi hapa Kwangu. Na kulinganisha wana na watu kwa wazaliwa wa kwanza, kweli ni tofauti kati ya mbinguni na dunia: Ingawa wana na watu ni bora zaidi kuwaliko

watendaji huduma, wao sio wale walio Wangu hata kidogo. Inaweza kusemekana pia kwamba wana na watu wanachaguliwa kwa kuongezea kutoka miongoni mwa wanadamu. Kwa hivyo daima Nimelenga nguvu Yangu kwa wazaliwa wa kwanza, na kisha Nitawaacha wazaliwa wa kwanza wawakamilishe hawa wana na watu. Hizi ndizo hatua za baadaye za kazi Yangu. Sasa hakuna haja kuwaambia, kwa hivyo Nimelitaja mara chache kwa wana na watu, lakini ni kwa wazaliwa wa kwanza pekee ndiyo Nimesema kwa kurudia na kutaja mambo haya kwa kurudia. Hivi ndivyo Ninavyosema na kufanya kazi. Hakuna mtu anayeweza kubadili hili—Mimi pekee ndiye Nina uamuzi wa mwisho kuhusu kila kitu.

Kila siku Narudisha mapigo dhidi ya dhana zenu, kila siku Namchambua kila mmoja wenu. Wakati ambapo Nimesema hadi mahali fulani, mnarudia hali mbaya na tena mnatenganisha ubinadamu Wangu kutoka kwa uungu Wangu. Wakati huu muda umefika wa watu kufichuliwa: Watu hufikiri kwamba bado Naishi katika nyama na Mimi si Mungu Mwenyewe hata kidogo, kwamba Mimi bado ni mwanadamu na Mungu bado ni Mungu, na kwamba Mungu hana uhusiano wowote na mtu Niliye Mimi. Binadamu hawa ni wapotovu jinsi gani! Nimezungumza awali maneno mengi sana, ambayo mmechukulia kutoka kitambo kama kwamba hayakuwepo, kiasi kwamba linanifanya kuwachukia sana, linanifanya kuwakirihi! Mimi—Mungu Mwenyewe kamili—ubinadamu Wangu pamoja na uungu Wangu kamili, nani anayethubutu kunikosea kwa kawaida? Nani anathubutu kunipinga katika mawazo yake? Baada ya maafa Yangu makuu kuanza kushuka Nitawaadhibu mmoja mmoja, Sitamsamehe yeyote, ila badala yake kuwaadhibu wote vikali. Roho Wangu anafanya kazi binafsi. Hili halimaanishi kwamba Mimi si Mungu Mwenyewe; kinyume chake kabisa, linamaanisha zaidi kwamba Mimi ni Mungu Mwenyewe mwenye uweza. Watu hawaniujui—wote wananipinga na hawatazami kudura Yangu kutoka kwa maneno Yangu, lakini badala yake wanajaribu kupata kitu katika maneno Yangu ambacho wanaweza kutumia dhidi Yangu na kupata makosa Kwangu. Wakati ambapo siku moja Naonekana na wazaliwa Wangu wa kwanza Sayuni, Nitaanza kushughulikia mambo haya. Katika kipindi hiki Nafanya kazi hii kimsingi. Wakati ambapo Nimezungumza hadi kiwango fulani, idadi kubwa ya watendaji huduma itakuwa imerudi nyuma, na wazaliwa wa kwanza watakuwa pia wamepitia kila aina ya taabu. Kwa kuendelea kwa hatua hizi mbili za kazi, kazi Yangu itafika tamati. Wakati huo huo Nitawarudisha wazaliwa Wangu wa kwanza Sayuni. Hizi ndizo hatua za kazi Yangu.

Wazaliwa Wangu wa kwanza ni sehemu muhimu ya ufalme Wangu, ambayo kutoka kwayo kunaweza kuonekana kwamba nafsi Yangu ni ufalme—ufalme Wangu unazaliwa na kuzaliwa kwa wazaliwa Wangu wa kwanza. Kwa maneno mengine, ufalme Wangu umekuwepo tangu uumbaji wa dunia, na kuwapata wazaliwa Wangu wa kwanza (kumaanisha kuwapata tena wazaliwa Wangu wa kwanza) ni kufanya upya ufalme Wangu. Kutoka kwa hilo unaweza kuona

kwamba wazaliwa wa kwanza ni wa umuhimu maalum. Kama tu kuna wazaliwa Wangu wa kwanza, hapo ndipo kutakuwa na ufalme, basi uhalisi wa kutawala katika mamlaka utatimia, basi kutakuwa na maisha mapya, na basi enzi nzima nzee inaweza kukamilishwa. Mwelekeo huu hauepukiki. Kwa sababu wazaliwa wa kwanza wako katika nafasi hii—kwa sababu wazaliwa wa kwanza wanaashiria uharibifu wa dunia, uangamizaji wa Shetani, kufichuliwa kwa tabia halisi ya watendaji huduma, kwamba joka kubwa jekundu halitakuwa na uzao na liashuka katika ziwa la moto na kibiriti—kwa hivyo wale wanaoshikilia madaraka na wale ambao ni uzao wa joka kubwa jekundu wanazuia kwa kurudia, wanapinga kwa kurudia, na wanaharibu kwa kurudia. Lakini Nawapandisha cheo kwa kurudia, Nawashuhudia kwa kurudia, na kuwafichua wazaliwa Wangu wa kwanza kwa kurudia. Kwa kuwa wale tu ambao wametoka Kwangu ndio wanafaa kunitolea ushuhuda; ni wao pekee ndio wana sifa zinazostahili kuishi kwa kunidhihirisha, na ni wao pekee ndio wana msingi wa kupigana vitani na kushinda ushindi mzuri kwa ajili Yangu. Wale ambao wametengana na Mimi ni udongo mdogo wa mfinyanzi mkononi Mwangu pekee—viumbe walioumbwa, kila moja wavyo. Wale ambao ni wana na watu ni walio bora waliochaguliwa kutoka kwa viumbe wa uumbaji, lakini si Wangu. Kwa hivyo, kuna tofauti kubwa kati ya wazaliwa wa kwanza na wana. Wana hawastahili kulinganishwa na wazaliwa wa kwanza hata kidogo—wanatawaliwa na kuongozwa na wazaliwa wa kwanza. Sasa mnapaswa kuwa wazi kabisa kuhusu hili! Kila neno ambalo Nimesema ni kweli, na si uongo hata kidogo. Yote haya ni sehemu ya maonyesho ya nafsi Yangu, na ni tamko Langu.

Nimesema Siongei mambo matupu, na Sifanyi makosa, ambalo linatosha kuonyesha uadhama Wangu. Lakini watu hawawezi kujua tofauti kati ya mema na mabaya, na ni wakati kuadibu Kwangu kunawafikia tu ambapo wanaridhishwa kikamilifu; vinginevyo wanabaki waasi na wakaidi, kwa hivyo hii ndiyo maana Natumia kuadibu kurudisha mapigo dhidi ya wanadamu wote. Katika dhana ya binadamu, kwa kuwa kuna Mungu Mwenyewe pekee, kwa nini kuna wazaliwa wengi wa kwanza wanaotoka Kwangu? Naweza kulisema kwa njia hii: Kutokana na shughuli Zangu mwenyewe, Nasema kile Nilicho tayari kusema, kwa hivyo watu wanaweza kunifanyia nini? Naweza pia kulisema kwa njia hii: Ingawa Mimi na wazaliwa wa kwanza si wa mfano mmoja, sisi ni wa Roho mmoja, kwa hivyo wote wanaweza kufanya kazi kwa pamoja nami. Sisi si wa mfano mmoja ili kuruhusu watu wote kuweza kuona kila sehemu ya nafsi Yangu kwa uwazi usio wa kawaida kabisa, kwa hivyo Nawaacha wazaliwa Wangu wa kwanza wawe na mamlaka pamoja na Mimi juu ya mataifa yote na watu wote. Huu ndio mfumo wa amri Zangu za utawala (mfumo Ninaozungumzia unamaanisha kwamba sauti Yangu ni pole na Naanza kuzungumza kwa wana na watu). Watu wengi wana mashaka kuhusu kipengele hiki, lakini hawapaswi kuwa na shaka sana. Nitafichua fikira zote za watu moja baada ya nyingine, kwa nia ya kuwafanya watu wahisi aibu wasiwe na pahali pa kujificha. Nasafiri kote ulimwenguni hadi

miisho ya dunia na kutazama uso mzima wa ulimwengu. Nachunguza kila aina ya mtu—hakuna mtu ambaye anaweza kuhepa udhibiti Wangu. Nashiriki katika kila aina ya kitu, na hakuna kitu ambacho Sishughulikii binafsi. Nani anayethubutu kukana kudura Yangu? Ni nani anayethubutu kutoridhika kikamilifu kunihusu? Nani anayethubutu kutosujudu kikamilifu mbele Yangu? Mbingu zote zitabadilika kwa sababu ya wazaliwa Wangu wa kwanza, na hata zaidi, dunia nzima itatetemeka kwa nguvu nyingi kwa sababu ya Mimi na wazaliwa Wangu wa kwanza. Watu wote watapiga magoti mbele ya nafsi Yangu, na vitu vyote hakika vitakuja katika udhibiti wa mikono Yangu—bila kosa hata kidogo. Kila mtu lazima aridhike kikamilifu na kila kitu kitakuja nyumbani Mwangu na kunitolea huduma. Hii ndiyo sehemu ya mwisho ya amri Zangu za utawala. Kuanzia sasa kuendelea kila makala ya amri Zangu za utawala, kikilenga watu tofauti, kitaanza kuzaa matunda? (Kwa sababu amri Zangu za utawala zinatolewa kwa umma kikamilifu, na kwa kila aina ya mtu na kila kitu matayarisho ya kufaa yamefanywa. Watu wote watakuwa katika mahala pao pa kufaa na tabia halisi ya kila aina ya mtu itafichuliwa kwa sababu ya amri Zangu za utawala). Huku ndiko kufika kwa amri za utawala zilizo kweli na halisi.

Sasa, kwa mujibu wa hatua za kazi Yangu, Ninasema ninachotaka kukisema, na kila mtu lazima akichukulie kwa uzito. Kotekote katika enzi, kinywa cha kila mtakatifu kimetaja “Yerusalemu Mpya,” na kila mtu anaujua, lakini hakuna mtu anaelewa maana ya kweli ya neno hili. Kwa kuwa kazi ya leo imeendelea hadi kwa hatua hii, Nitafichua maana ya kweli ya neno hili kwenu kuwafanya mlielewe. Lakini Nina mpaka—bila kujali jinsi Ninavyolielezea na bila kujali jinsi Ninavyolisema kwa uwazi, hamwezi kulielewa kabisa kwa sababu hakuna mtu anayeweza kupata uhalisi wa neno hili. Zamani kile ambacho Yerusalemu ilirejelea kilikuwa makao Yangu duniani, yaani, mahali ambapo Natembea na kusonga. Lakini neno “mpya” linabadilisha neno hili na si sawa hata kidogo. Watu hawawezi kulielewa hata kidogo. Watu wengine wanafikiri linarejelea ufalme Wangu; watu wengine wanafikiri ni mwanadamu Niliye; watu wengine wanafikiri ni mbingu mpya na dunia mpya; na watu wengine wanafikiri ni dunia mpya baada ya Mimi kuharibu dunia hii. Hata kama akili ya mtu inafikiri kwa wingi, na hata kama akili ya mtu ni changamani mno, bado hawezi kuelewa chochote kulihusu. Kotekote katika enzi, watu wamekuwa wakitumaini kujua au kuona maana ya kweli ya neno hili, lakini matamainio yao hayajawahi kutimizwa—wote wamevunjika matumaini na wamefariki, wakiacha matumaini yao nyuma; kwa sababu wakati Wangu ulikuwa haujafika bado Singeweza kumwambia mtu yeyote kwa urahisi. Kwa kuwa kazi Yangu imefanywa hadi kwa hatua hii Nitawaambia kila kitu. Yerusalemu Mpya unajumuisha haya mambo manne: ghadhabu Yangu, amri Zangu za utawala, ufalme Wangu na baraka zisizoisha Ninazowapa wazaliwa Wangu wa kwanza. Sababu ya Mimi kutumia neno “mpya” ni kwa sababu hizi sehemu nne ni sehemu zilizofichwa. Kwa sababu hakuna mtu anayejua ghadhabu Yangu, hakuna mtu anayejua amri

Zangu za utawala, hakuna mtu ambaye ameona ufalme Wangu, na hakuna mtu ambaye amefurahia baraka Zangu, “mpya” linarejelea kile ambacho kimefichwa. Hakuna mtu anayeweza kuelewa kikamilifu kile ambacho Nimesema, kwa sababu Yerusalemu Mpya umeshuka duniani lakini hakuna mtu amepitia uhalisi wa Yerusalemu Mpya mwenyewe. Bila kujali jinsi Ninavyouzungumzia kwa ukamilifu, watu hawataelewa kwa ukamilifu. Hata kama mtu anaelewa, ni maneno yake, ni akili yake, na ni dhana zake. Huu ni mwelekeo usioepukika, ni njia ya pekee, ambayo hakuna mtu anaweza kuhepa.

Sura ya 113

Hekima Yangu iko ndani ya kila kitendo Ninachokifanya, lakini mwanadamu hawezi kabisa kuelewa hekima hii; mwanadamu anaweza tu kuona matendo Yangu na maneno Yangu, si utukufu Wangu au kuonekana kwa nafsi Yangu, kwa kuwa mwanadamu kimsingi hana uwezo huu. Hivyo, bila Mimi kumbadilisha mwanadamu, wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi tutarejea Sayuni na kubadili sura, ili mwanadamu aweze kuiona hekima Yangu na nguvu Yangu yote. Hekima na kudura Yangu yote ambayo mwanadamu anaiona sasa, ni sehemu tu moja ndogo ya utukufu Wangu, isiyostahili kutajwa kamwe. Kutoka kwahili, inaweza kuonekana kwamba hekima Yangu na utukufu Wangu havina kikomo—yenye kina sana—ina akili ya mwanadamu kimsingi haina uwezo wa kuuzingatia au kuelewa. Kuujenga ufalme ni wajibu wa wazaliwa wa kwanza, na hii ni kazi Yangu pia. Hiyo ni kusema, ni kipengele cha mpango Wangu wa usimamizi. Ujenzi wa ufalme si sawa na ujenzi wa kanisa; kwa kuwa wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi ni nafsi Yangu na ufalme, basi wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi tutakapoingia katika Mlima Sayuni, ujenzi wa ufalme utakuwa umetimia. Kusema kwa njia nyingine, ujenzi wa ufalme ni hatua katika kazi—hatua ya kuingia katika ulimwengu wa kiroho. (Hata hivyo, yote ambayo Nimefanya tangu kuiumba dunia yamekuwa kwa ajili ya hatua hii. Ingawa Nasema ni hatua, kwa kweli si hatua kabisa.) Hivyo, Nawatumia watendaji huduma wote wa hatua hii, na kwa sababu hiyo, katika siku za mwisho, idadi kubwa za watu itajiondoa; wote wanatoa huduma kwa wazaliwa wa kwanza. Yeyote anayetoa wema kwa watendaji huduma hawa ataaga kutokana na laana Zangu. (Watendaji huduma wote wanawakilisha njama za joka kubwa jekundu, na wote ni watumishi wa Shetani, kwa hiyo wale ambao wanaeneza wema kwa watu hawa ni vikaragosi wa joka kubwa jekundu nao ni wa Shetani.) Napenda yote ambayo Ninapenda, na Nachukia walengwa wote wa laana Zangu na kuteketezwa. Je, ninyi pia mnaweza kufanya hivi? Bila shaka Sitamsamehe Yeyote anayesimama dhidi Yangu, wala kumwachilia huru! Kwa kufanya kila tendo, Ninapanga kwa idadi kubwa ya watendaji huduma kunihudumia Mimi. Hivyo inaweza kuonekana kwamba katika historia nzima, imekuwa kwa ajili ya hatua hii ya leo ambapo manabii na mitume wote wametoa huduma, na hawajishughulishi na kuutafuta moyo Wangu, hawatoki Kwangu. (Ingawa wengi wao ni

waaminifu Kwangu, hakuna aliye Wangu. Hivyo, kukimbia kwao huku na kule ni kuunda msingi wa hatua hii ya mwisho kwa ajili Yangu, lakini jitihada zao zote ni bure kuhusiana na wao wenyewe). Kwa hiyo, katika siku za mwisho hata zaidi kutakuwa na idadi kubwa za watu wa kujiondoa. (Sababu Ninasema “idadi kubwa” ni kwamba mpango Wangu wa uongozi umefikia kilele, ujenzi wa ufalme Wangu umefanikiwa, na wazaliwa wa kwanza wameketi juu ya kiti cha enzi.) Yote hayo ni kutokana na kuonekana kwa wazaliwa wa kwanza. Kwa sababu wazaliwa wa kwanza wameonekana, joka kubwa jekundu hujaribu kila njia iwezekanayo kutekeleza uharibifu na kutumia njia zote. Linatuma kila aina ya pepo wabaya ambao huja kufanya huduma kwa ajili Yangu, ambao wamebainisha tabia zao halisi zilivyo katika wakati wa sasa, na ambao wamejaribu kukatiza usimamizi Wangu. Haya hayawezi kuonekana kwa macho; yote ni mambo ya ulimwengu wa kiroho. Hivyo, watu hawaamini kwamba kutakuwa na idadi kubwa za watu ambao hurudi nyuma, ilihali Najua yale Ninayofanya, Ninaelewa usimamizi Wangu; hii ndiyo sababu ya kutomruhusu mwanadamu kuingilia kati. (Kutakuja siku ambapo kila aina ya pepo mbaya asiye faa atafichua nafsi yake ya kweli, na watu wote wataridhika kwa dhati.)

Nawapenda wazaliwa Wangu wa kwanza, lakini wale ambao ni ukoo wa joka kubwa jekundu na wanaonipenda kwa uaminifu mkubwa, Siwapendi kabisa; kwa kweli Nawadharau hata zaidi. (Watu hawa si Wangu, na ingawa wanadhihirisha nia nzuri, na kunena maneno ya kufurahisha, hii yote ni njama ya joka kubwa jekundu, na hivyo Nawachukia hadi kwa moyo Wangu wote.) Hii ni tabia Yangu, na huu ni ukamilifu Wangu kwa ukamilifu. Mwanadamu hawezi kuelewa kabisa. Kwa nini ukamilifu wa haki Yangu unafichuliwa hapa? Kutokana na hili, mtu anaweza kutambua tabia Yangu takatifu na isiyoruhusu kosa lolote. Naweza kuwapenda wazaliwa Wangu wa kwanza na kuwadharau wale wote ambao si wazaliwa Wangu wa kwanza (hata ikiwa wao ni watu waaminifu). Hii ni tabia Yangu. Je, hamwezi kuona? Katika fikira za watu, Mimi daima ni Mungu mwenye huruma, nami Nawapenda wote wanaonipenda; je, tafsiri hii si kukufuru dhidi Yangu Mimi? Naweza kuwapenda wanyama na fahali? Naweza kumchukua Shetani kama mzaliwa Wangu wa kwanza na kufurahia hilo? Upuuzi! Kazi Yangu inatekelezwa kuwahusu wazaliwa Wangu wa kwanza, na mbali na wazaliwa Wangu wa kwanza, Sina kitu kingine cha kupenda. (Wana na watu ni nyongeza, lakini si muhimu.) Watu wanasema kwamba hapo awali, Nilifanya kazi nyingi sana isiyo na maana, lakini kwa maoni Yangu, kwa kweli kazi hiyo ilikuwa ya thamani sana, na yenye maana sana. (Hii inarejelea kikamilifu kazi yote iliyofanyika wakati wa kuupata mwili kuwili; kwa sababu Nataka kufichua nguvu Zangu, lazima Niwe mwili ili Niikamilishe kazi Yangu.) Sababu Ninasema Roho Wangu huja kufanya kazi yeye binafsi, ni kwamba kazi Yangu ikamilishwe katika mwili. Hiyo ni kusema, wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi sasa tunaanza kuingia katika mapumziko. Vita na Shetani katika mwili ni vikali zaidi kuliko vita na Shetani katika ulimwengu wa kiroho, vinaweza kuonekana na

watu wote, hivyo hata ukoo wa Shetani pia wnaweza kutoa ushuhuda mzuri kwa ajili Yangu, na huna nia ya kuondoka; hii ndiyo maana yenyewe ya kufanya Kwangu kazi katika mwili. Ni hasa ili kuufanya ukoo wa ibilisi umuaibishe ibilisi mwenyewe; hii ni aibu kubwa sana kwa ibilisi Shetani, kubwa sana kiasi kwamba hana mahali pa kuficha aibu yake, na kuomba rehema mbele Zangu kwa kurudia rudia. Nimeshinda, Nimeshinda juu ya kila kitu, Nimeipenya mbingu ya tatu na kuufikia Mlima Sayuni, kufurahia neema ya kifamilia pamoja na wazaliwa Wangu wa kwanza, milele kufurahia sanakatika karamu kubwa ya ufalme wa mbinguni!

Kwa wazaliwa wa kwanza, Nimelipa kila gharama na kuchukua maumivu yote kwa juhudi zangu. (Mwanadamu hajui kabisa kwamba yote Nimefanya, yote Nimesema, ukweli kwamba Nabaini kila aina ya pepo mbaya, na kwamba Nimemfukuza kila aina ya mtendaji huduma,—hii yote imekuwa kwa sababu ya wazaliwa wa kwanza.) Lakini ndani ya kazi nyingi, mpango Wangu ni wenye utaratibu; kazi hii haifanywi ovyo. Katika matamshi Yangu kila siku, mnapaswa kuweza kuona mbinu na hatua za kazi Yangu na hatua zake; katika matendo Yangu kila siku mnapaswa kuona hekima Yangu na kanuni Zangu katika kukabiliana na mambo. Kama Nilivyosema, Shetani amewatuma wale ambao wananifanyia huduma kwa nia ya kukatiza usimamizi Wangu. Hawa watendaji huduma ni magugu, lakini neno “ngano” hairejelei wazaliwa wa kwanza, lakini kwa wana wote na watu ambao si wazaliwa wa kwanza. “Siku zote ngano itakuwa ngano, siku zote magugu yatakuwa magugu”; hii ina maana asili ya wale ambao ni wa Shetani haiwezi kubadilika kamwe. Kwa hiyo, kwa ufupi, wao wanabaki Shetani. “Ngano” linarejelea wana na watu, kwa sababu Niliweka ubora Wangu ndani ya watu hawa kabla ya kuumbwa ulimwengu. Kwa sababu Nimeshasema tayari kwamba asili ya mwanadamu haibadiliki, na hiyo ndiyo maana ngano siku zote itakuwa ngano. Basi, wazaliwa wa kwanza ni nini? Wazaliwa wa kwanza wanatoka Kwangu, hawaumbwi nami, hivyo hawawezi kuitwa ngano (kwa sababu kutajwa kwa aina yoyote kwa ngano, daima kumeunganishwa na maneno “kupanda,” na “kupanda” maana yake ni “kuumba”; magugu yote yamepandwa na Shetani kisiri, ili kutenda kama watendaji huduma). Mtu anaweza tu kusema kwamba wazaliwa wa kwanza ni onyesho kamili na karimu la nafsi Yangu, wanapaswa kuwakilishwa na dhahabu na fedha, na vito vya thamani. Hili linagusia ukweli kwamba kuja Kwangu ni kama kule kwa mwizi, nami Nimekuja kuiba dhahabu na fedha na vito vya thamani (kwa sababu hii dhahabu na fedha na vito vya thamani vyote vilikuwa Vyangu, nami Nataka kuvirudisha nyumbani Kwangu). Wakati ambapo wazaliwa wa kwanza nami tutarudi Sayuni pamoja, hii dhahabu, hii fedha na vito vya thamani vitakuwa vimeibiwa na Mimi. Wakati huu, kutakuwa na vizuizi na vurugu ya Shetani, na hivyo Nitazichukua dhahabu, fedha na vito vya thamani na kuzindua vita vya maamuzi na Shetani. (Hapa, bila shaka sisemi hadithi; hili ni tukio katika ulimwengu wa kiroho, hivyo watu hawana uwazi kabisa kulihusu, na wanaweza tu kulisikia kama hadithi. Lakini ni jukumu lenu

kuona kutoka katika maneno Yangu kile ambacho mpango Wangu wa usimamizi wa miaka elfu sita unahusu, na ni sharti msilichukulie kama utani kabisa. Vinginevyo, Roho Wangu Ataondoka kutoka ndani ya wanadamu wote.) Leo, vita hivi vimekamilika kabisa, nami Nitawaleta wazaliwa Wangu wa kwanza (Nikizileta dhahabu, fedha na vito vya thamani ambavyo ni Vyangu) pamoja nami Mlimani Kwangu Sayuni. Kutokana na uhaba wa dhahabu, fedha na vito vya thamani, na kwa sababu ya thamani yao, Shetani hujaribu kila namna iwezekanayo kuvipokonya, lakini Nasema tena na tena kwamba kile kitokacho Kwangu lazima kinirudie, maana yake ambayo imetajwa hapo juu. Msemo Wangu kwamba wazaliwa wa kwanza wanatoka Kwangu na ni Wangu ni tangazo kwa Shetani. Hakuna mtu anayeelewa hili, na kwa ukamilifu ni jambo ambalo hutokea katika ulimwengu wa kiroho. Hivyo, mwanadamu haelewi kwa nini Narudia kusisitiza kwa kurudia kwamba wazaliwa wa kwanza ni Wangu; leo, mnapaswa kuelewa! Nimesema kwamba maneno Yangu yana kusudi na hekima, lakini mnaelewa hili kwa nje—hakuna mtu hata mmoja anayeweza kuona hili wazi katika roho.

Nasema zaidi na zaidi, na zaidi Ninavyosema ndivyo makali zaidi maneno Yangu yanavyokuwa. Inapofika kiwango fulani, Nitayatumia maneno Yangu kuwafinyanga watu kwa kiwango fulani, kuwafanya watu wasiridhishwe moyoni na kwa neno tu, lakini zaidi ya hayo kuwafanya wakaribie kifo; hii ni mbinu Yangu ya kazi na jinsi kazi Yangu inavyoendelea kwa hatua zake. Lazima iwe hivyo; ni hivyo tu ndivyo inavyoweza kumwaibisha Shetani na kuwakamilisha wazaliwa wa kwanza (kuyatumia maneno Yangu ili hatimaye kuwafanya wazaliwa wa kwanza kamili, ili kuwaruhusu kujitenga na mwili na kuingia katika ulimwengu wa kiroho). Mwanadamu haelewi mbinu na sauti ya maneno Yangu. Utambuzi kiasi unafaa kuwajia nyote kutokana na maelezo Yangu na mnapaswa kufuata maneno Yangu ili muikamilishe kazi ambayo mnapaswa kuifanya. Hiki ndicho ambacho Nimewaaminia. Lazima mfahamu hili, na si tu kutoka ulimwengu ya nje, lakini muhimu zaidi, kutoka katika ulimwengu ya kiroho.

Sura ya 114

Niliumba ulimwengu dunia; Nilitengeneza milima, mito, na vitu vyote; Niliunda ulimwengu na miisho ya dunia; Niliwaongoza wana Wangu na watu Wangu; Niliamuru vitu na mambo yote. Sasa, Nitawaongoza wazaliwa Wangu wa kwanza warudi kwenye Mlima Wangu Sayuni, kurudi mahali ambapo Naishi, ambayo itakuwa hatua ya mwisho katika kazi Yangu. Yote ambayo Nimeyatenda (kila kitu kilichofanyika kutoka uumbaji mpaka sasa) yalikuwa kwa sababu ya hatua ya leo ya kazi Yangu, na zaidi ni kwa sababu ya utawala wa kesho, ufalme wa kesho, na kwa ajili ya Mimi na wazaliwa Wangu wa kwanza kuwa na furaha ya milele. Hili limekuwa lengo Langu katika kuumba vitu vyote na yatakuwa mafanikio Yangu ya mwisho wa uumbaji. Kuna kusudi na mpango kwa kile Ninachosema na kufanya; hakuna kinachofanyika ovyo ovyo.

Ingawa Ninasema kuwa na Mimi yote ni uhuru na haki ya kujiamulia la kufanya, hata hivyo kila kitu Ninachofanya ni chenye maadili, yote Ninayofanya yamewekwa kwa msingi wa hekima na tabia Yangu. Je, mmeona chochote kuhusu hili? Kuanzia uumbaji mpaka leo, kando na wazaliwa Wangu wa kwanza, hawapo ambao wamenijua Mimi na hawapo ambao wameuona uso Wangu wa kweli. Jambo la pekee Nililofanya kwa wazaliwa Wangu wa kwanza ni kwa sababu kimsingi wao ni sehemu ya nafsi Yangu.

Nilipoumba ulimwengu, Nilimtengeneza mwanadamu katika makundi manne ya safu kwa mujibu wa mahitaji Yangu, ambayo ni: wana Wangu, watu Wangu, wale wanaotoa huduma, na wale ambao wataangamizwa. Ni kwa nini wazaliwa Wangu wa kwanza hawako kati ya orodha hii? Ni kwa sababu wazaliwa Wangu wa kwanza si wa asili ya uumbaji; wanatoka Kwangu na sio wa wanadamu. Nilifanya mipango kwa ajili ya wazaliwa Wangu wa kwanza kabla Sijapata mwili; ni kaya gani ambayo wangezaliwa kwayo na ni akina nani wangekuwa huko kuwahudumia—vitu vyote hivi vilipangwa na Mimi. Nilipanga pia ni wakati upi ambapo ni yupi kati yao angepatwa tena na Mimi na mwishowe tutarudi Sayuni pamoja. Haya yote yalipangwa kabla ya uumbaji, kwa hivyo hakuna mtu anayejua jambo hilo na halijaandikwa katika kitabu chochote kwa sababu hayo ni mambo ya Sayuni. Zaidi ya hayo, Nilipopata mwili, Sikumpa mwanadamu welekevu huu, kwa hiyo hakuna mtu aliyejua mambo hayo. Mtakaporejea Sayuni, mtajua jinsi mlivyofanana zamani, jinsi mnavyofanana sasa, na kile ambacho mmefanya katika maisha haya. Hivi sasa ni kuwa tu Ninawaambieni mambo haya wazi na kidogo kidogo, vinginevyo hamngeelewa hata mfanye bidii namna gani, na mngezuia usimamizi Wangu. Leo, ingawa Nimejitenganisha kutokana na miili ya wengi wa wazaliwa Wangu wa kwanza, kwa suala la mwili, sisi tu wa Roho mmoja, na ingawa sura yetu ya mwili inaweza kuwa tofauti, sisi, tangu mwanzo hadi mwisho, tu Roho mmoja. Hata hivyo, dhuria ya Shetani haitatumia hii kama nafasi ya kunyonya. Haijalishi jinsi unavyojificha, inabakia ya juu juu, na Sitaiafiki. Kwa hiyo mtu anaweza kuona kutoka kwa hili kuwa wale ambao wanasisitiza mambo ya juu juu na kutafuta kuniiga kwa nje wana uhakika asilimia mia moja kuwa ni Shetani. Kwa sababu roho zao ni tofauti na wao si wa wapendwa Wangu, haijalishi wananiiga namna gani hawafanani na Mimi. Zaidi ya hayo, kwa kuwa kimsingi wazaliwa Wangu wa kwanza ni wa Roho moja pamoja nami, hata kama hawaniigi, wanasema na kutenda sawasawa na Mimi, na wote ni waaminifu, safi, na wazi (kwa wale ambao hawana hekima ni kwa sababu tu ya uzoefu wao mdogo ulimwenguni, na hivyo kukosa hekima si dosari ya wazaliwa Wangu wa kwanza; wakati ambapo watarudi katika mwili yote yatakuwa sawa). Kwa hiyo ni kwa sababu iliyoelezwa hapo awali kuwa watu wengi bado hawabadili asili yao ya kale bila kujali namna Ninavyowashughulikia. Lakini kwa wazaliwa Wangu wa kwanza, wanakubali makusudi Yangu bila Mimi kulazimika kuwashughulikia na hii ni kwa sababu sisi ni wa Roho mmoja. Wanahisi ndani ya roho zao nia

ya kujitumia kabisa kwa ajili Yangu. Kwa hiyo mbali na wazaliwa Wangu wa kwanza, hakuna mtu ambaye anajali kwa kweli na kwa dhati makusudi Yangu; ni baada tu ya Mimi kumshinda Shetani ndiyo wako tayari kunifanyia huduma.

Hekima Yangu na wazaliwa Wangu wa kwanza husimama juu ya yote, hushinda yote, na hakuna kitu au mtu au jambo linalothubutu kuwazuia. Zaidi ya hayo, hakuna mtu, jambo, au kitu ambacho kinaweza kuwashinda, na badala yake yote yanajisalimisha kwa utii mbele ya nafsi Yangu. Huu ni ukweli ambao unatokea mbele ya macho ya mtu na ukweli ambao tayari Nimekwisha kuutimiza. Yeyote anayeng'ang'ania kutotii (wale wasiotii bado wanamtaja Shetani na wale wanaomilikiwa na Shetani bila shaka ni Shetani), kwa hakika Nitawaangamiza kabisa ili kusiwe na shida ya baadaye; watakufa mara moja kutokana na kuadibu Kwangu. Aina hii ya Shetani ni wale ambao hawana nia ya kutoa huduma Kwangu na vitu hivi daima vimenipinga kwa ukaidi tangu uumbaji, na leo vinang'ang'ania kutonitii (watu hawawezi kuona hili kwa sababu ni jambo linalohusu roho tu. Mtu wa aina hii anawakilisha Shetani wa aina hii). Nitawaangamiza kwanza kabla kitu kingine chochote kiwe tayari, Nikiwafanya wapokee adhabu kali milele (“kuangamiza” hapa hakumaanishi kutokuwepo tena, lakini badala yake kunamaanisha kiwango cha ukatili ambacho watapitia, na neno “kuangamiza” hapa ni tofauti na neno “kuangamiza” linalotumika kwa wale ambao wataangamizwa), na watalia na kusaga meno milele na milele, bila kikomo. Mwanadamu hawezi kufikiria mandhari hayo kwa vyovyote. Kwa mawazo ya wanadamu yenye kufa, hawawezi kufahamu mambo ya kiroho, kwa hivyo, mtaelewa mambo mengi zaidi baada ya kurudi Sayuni tu.

Katika nyumba Yangu ya baadaye, hakutakuwa na yeyote isipokuwa wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi na wakati huo tu ndipo lengo Langu litafikiwa na mpango Wangu utazaa matunda, kwa kuwa yote yatarejeshwa kwa hali yake ya awali na yote yataainishwa kulingana na mfano wake. Wazaliwa Wangu wa kwanza watakuwa Wangu, wana Wangu na watu watakuwa miongoni mwa viumbe na watendaji huduma na wale walioangamizwa watakuwa wa Shetani. Baada ya kuuhukumu ulimwengu, Mimi na wazaliwa Wangu wa kwanza tutaanza tena maisha ya kiungu na hawataniacha kamwe na daima watakuwa pamoja na Mimi. Siri zote ambazo zinaweza kueleweka na akili za kibinadamu zitafichuliwa kwenu kidogo kidogo. Katika historia yote, kumekuwa na watu wengi ambao wameuawa kishahidi kwa sababu Yangu, wakijitolea kikamilifu Kwangu, lakini wanadamu ni viumbe hata hivyo na haijalishi ni wazuri namna gani, hawawezi kuainishwa kama Mungu; huu ni mwenendo usioepukika na hauwezi kubadilishwa na mtu yeyote. Hata hivyo, ni Mungu ambaye Anaumba vitu vyote na watu ni viumbe, na Shetani ni, hata hivyo, anayelengwa kwa uharibifu na adui Wangu wa kuchukiwa—hii ndio maana ya kweli zaidi ya maneno “ijapokuwa milima na mito yaweza kuhama na kubadilika, asili ya mtu haitabadilika.” Kuwa katika hali hii na hatua hii sasa ni ishara kwamba Mimi na wazaliwa

Wangu wa kwanza tutaingia katika pumziko. Hii ni kwa sababu kazi Yangu katika ulimwengu imekamili kabisa na hatua inayofuata ya kazi Yangu itanihitaji Nirudi kwenye mwili kuikamilisha. Hizi ni hatua za kazi Yangu na Nilizipanga vizuri zamani. Hoja hii inapaswa kuonekana wazi, vinginevyo watu wengi watakiuka amri Zangu za utawala.

Sura ya 115

Kwa sababu yako, Moyo Wangu utakufurahia sana; kwa sababu yako, mkono Wangu utacheza kwa furaha juu yako, na Nitakupa baraka zisizo na mwisho, kwa kuwa kabla ya uumbaji, ulitoka Kwangu, na leo lazima urejee upande Wangu, kwa kuwa wewe si wa dunia ama ulimwengu bali, badala yake, wewe ni Wangu. Nitakupenda milele, Nitakubariki milele na Nitakulinda milele. Ni wale tu ambao wametoka Kwangu wanaoyajua mapenzi Yangu, na ni wao tu wataudhukuru mzigo Wangu na kufanya kile ambacho Ninataka kukifanya. Sasa, kila kitu tayari kimekwisha kutimizwa. Moyo Wangu ni kama mpira wa moto, ukiwaonea shauku wana Wangu wapendwa kuunganishwa tena nami hivi punde, ukitamani sana nafsi Yangu kurejea Sayuni kikamilifu hivi karibuni. Una ufahamu kiasi juu ya hili. Ingawa mara nyingi hatuwezi kufuatana katika roho, mara nyingi tunaweza kuandamana katika roho na kukutana katika mwili. Baba na wana daima hawatenganiki, wanaunganishwa kwa urafiki wa karibu sana. Hakuna anayeweza kukutoa katika upande Wangu hadi siku ya kurudi katika Mlima Sayuni. Ninawapenda wazaliwa Wangu wote wa kwanza wanaotoka Kwangu na Ninawachukia maadui wote wanaonipinga. Nitawarudisha wale Ninaowapenda Sayuni na kuwatupa wale wote Ninaowachukia kuzimuni, katika jehanamu. Hii ndiyo kanuni kuu ya amri Zangu za utawala. Kila kitu ambacho wazaliwa Wangu wa kwanza husema au kutenda ni maonyesho ya Roho Wangu. Kila mtu lazima awe na ushuhuda kwa wazaliwa Wangu wa kwanza kwa ufahamu dhahiri juu yake. Hii ndiyo hatua inayofuata ya kazi Yangu, mtu yeyote akipinga, Nitawaomba wazaliwa Wangu wa kwanza kuwashughulikia. Ni tofauti sasa. Wale Ninaowapenda wakinena neno la hukumu, Shetani atakufa mara moja huko kuzimuni kwa sababu tayari Nimewapa mamlaka wazaliwa Wangu wa kwanza. Hii ni kusema kuwa kuanzia sasa kuendelea, ni wakati wa wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi kutawala kwa pamoja. (Hili ni katika awamu ya nyama. ambayo ni tofauti kidogo na kutawala pamoja katika mwili.) Yeyote anayeasi katika fikira atapitia hatima sawa na wale ambao hupinga mtu Niliye. Wazaliwa Wangu wa kwanza wanapaswa kutendewa jinsi Ninavyotendewa kwa sababu sisi tu wa mwili mmoja na hatuwezi kutenganishwa asilani. Leo wazaliwa Wangu wa kwanza wanapaswa kushuhudiwa kama Nilivyoshuhudiwa hapo zamani. Hii ni mojawapo ya amri Zangu za utawala; kila mtu lazima asimame na kuwa na ushuhuda.

Ufalme Wangu huenea hadi miisho ya dunia, wazaliwa Wangu wa kwanza husafiri hadi

miisho ya dunia na Mimi. Kuna vitu vingi ambavyo Mimi huvizungumzia ambavyo hamvielewi kwa sababu ya vipingamizi vya mwili wenu hivyo zaidi ya nusu ya kazi lazima ifanywe baada ya kurudi Sayuni. Inaweza kuonekana kutoka katika maneno Yangu kuwa hili haliko mbali sana, liko karibu kutimia. Kwa hivyo tena na tena Ninazungumza juu ya Sayuni na masuala katika Sayuni. Je, mnajua nia ya maneno Yangu ni gani? Je, mnajua ni nini kilicho ndani ya moyo Wangu? Moyo Wangu unatamani sana kurudi Sayuni punde, kutamatisha enzi nzima ya kale, kumaliza maisha yetu duniani (kwa kuwa Ninachukizwa sana na watu, mambo, vitu vya dunia, na kuchukia maisha katika mwili hata zaidi, na vizuizi vya mwili ni vikuu na kila kitu kitakuwa na usitawi baada ya kurudi Sayuni tu), na kupata tena maisha yetu katika ufalme. Madhumuni ya kupata mwili Kwangu mara ya kwanza yalikuwa kuweka msingi kwa ajili ya kupata mwili Kwangu mara ya pili. Hii ilikuwa njia ambayo ilipaswa kusafiriwa. Ni katika kujipeana kikamilifu kwa Shetani tu, ndipo Ningeweza kuwakomboa kuingia katika mwili Wangu wakati wa hatua ya mwisho. (Kama si kupitia kupata mwili Kwangu mara ya kwanza, Nisingeweza kutukuzwa, Nisingeweza kuchukua tena sadaka ya dhambi, hivyo mngekuja duniani kama wenye dhambi.) Kwa kuwa Nina hekima isiyo na kikomo, maadam Niliwaongoza kutoka Sayuni, Nitahakikisha Kuwarejesha Sayuni. Majaribio ya Shetani ya kuweka kizuizi njiani hayatafaulu kwa sababu kazi Yangu kuu ilitimizwa zamani sana. Wazaliwa Wangu wa kwanza ni sawa na Mimi, wao ni watakatifu na hawana mawaa na hivyo bado Nitarudi Sayuni pamoja na wazaliwa Wangu wa kwanza na hatutatengana daima.

Mpango Wangu mzima wa usimamizi unafichuliwa kwenu polepole. Nimeanza kutekeleza kazi Yangu katika mataifa yote miongoni mwa watu wote. Hili limetosha kuthibitisha kuwa wakati Nitakaporudi Sayuni hauko mbali sana kwa sababu kutekeleza kazi Yangu katika mataifa yote na miongoni mwa watu ni kitu ambacho kitafanywa baada ya kurejea Sayuni. Mwendo Wangu unaanza kupata kasi zaidi na zaidi. (Kwa kuwa siku ambapo Nitarudi Sayuni inawadia, Nataka kumaliza kazi Yangu duniani kabla Nirudi.) Nazidi kushughulika zaidi na zaidi na kazi Yangu na ilhali kuna kazi kidogo zaidi na zaidi Mimi kufanya duniani, nusra iwe haipo kabisa. (Kuwa na kazi Kwangu kunaelekezwa kwa kazi katika Roho, ambayo haiwezi kuonekana na mwanadamu kwa macho ila inaweza kupatika kidogo tu kutoka katika maneno Yangu; Kujishughulisha Kwangu sio kama ilivyo kuwa na shughuli katika mwili, bali kunaashiria kupanga Kwangu kwa kazi nyingi. Hii ni kwa sababu, kama ambavyo Nimesema, kazi Yangu duniani tayari imekwisha kumalizwa kikamilifu na kazi Yangu iliyobaki lazima isubiri hadi Nirejee Sayuni. (Sababu ya kuwa lazima Nirudi Sayuni ili kufanya kazi ni kuwa kazi ya baadaye haiwezi kutimizwa ndani ya mwili na iwapo kazi hizi zingefanywa katika mwili, ingeleta fedheha kwa jina Langu.) Wakati ambapo Nitawashinda maadui Wangu na kurudi Sayuni, maisha yatakuwa mazuri zaidi na yenye amani kuliko maisha ya kabla ya enzi. (Hii ni kwa

sababu Nimeshinda dunia kabisa, na kwa usaidizi wa kupata mwili Kwangu mara ya kwanza na kupata mwili Kwangu mara ya pili Nimetukuzwa kabisa. Katika kupata mwili Kwangu mara ya kwanza, Nilitukuzwa kwa sehemu tu lakini, katika kupata mwili Kwangu mara pili, nafsi Yangu inatukuzwa kabisa, na hivyo hakuna nafasi nyingine tena za Shetani kutumia. Kwa hivyo, maisha ya baadaye Sayuni yatakuwa mazuri na yenye amani hata zaidi.) Nafsi Yangu itaonekana kwa utukufu hata zaidi mbele ya dunia na Shetani ili kulifedhehesha joka kuu jekundu, hiki ndicho kiini cha hekima Yangu yote. Kadiri Ninavyozidi kuzungumzia vitu vya nje, ndivyo mnavyoweza kuelewa zaidi; kadiri Ninavyozungumzia vitu vya Sayuni ambavyo wanadamu hawawezi kuviona, ndivyo mtakavyofikiri zaidi kuwa vitu hivi ni bure na ndivyo itakavyokuwa vigumu zaidi kwenu kuviwazia, na mtafikiri kuwa Ninawaeleza hadithi za vichimbakazi. Hata hivyo, lazima muwe waangalifu, hamna maneno matupu kinywani Mwangu, maneno yanayotoka kinywani Mwangu ni maaminifu. Ingawa ni vigumu kuyaelewa kwa njia yenu ya kufikiri, hii ni kweli kabisa. (Kwa sababu ya udhaifu wa mwili, wanadamu hawawezi kuelewa kabisa na kikamilifu kile Ninachosema, na mambo mengi ambayo Nimesema Sijayafichua kabisa, lakini tutakaporejea Sayuni, Sitahitaji kuelezea, mtakuwa na ufahamu kwa kawaida.) Hii inapaswa kuchukuliwa kwa uzito.

Ingawa wanadamu wana upungufu wa mwili na dhana, bado Nataka kuyaimarisha mawazo yenu ya kufisha na kupigana dhidi ya dhana zenu kwa njia ya mafumbo yaliyofichuliwa kwa sababu Nimesema mara nyingi kwamba hii ni hatua ya kazi Yangu (kazi hii haitakoma hadi katika kuingia Sayuni). Kuna Mlima Sayuni akilini mwa kila mtu na ni tofauti kwa kila mtu. Kwa kuwa Ninaendelea kutaja Mlima Sayuni, Nitawaambia maelezo ya jumla juu yake ili mweze kuujua kidogo. Kuwa juu ya Mlima Sayuni ni kurudi katika dunia ya kiroho. Ingawa inahusu dunia ya kiroho, si pahali ambapo watu hawawezi kuona wala kugusa; hii inahusika na mwili. Sio usioonekana kabisa au usioshikika kwa sababu wakati ambapo mwili unaonekana una sura na umbo lakini wakati ambapo mwili hauonekani hauna sura au umbo. Katika Mlima Sayuni, hakutakuwa na wasiwasi juu ya chakula, nguo, mahitaji ya kila siku na makazi, wala hakutakuwa na ndoa au familia na hakutakuwa na mgawanyiko wa jinsia (wote walio juu ya Mlima Sayuni ni nafsi Yangu, wako katika mwili mmoja, kwa hivyo hakuna ndoa, familia au mgawanyiko wa jinsia), na kila kitu ambacho nafsi Yangu huzungumzia kitafanyika. Wakati ambapo watu hawajihadhari, nafsi Yangu itaonekana kati yao na wakati ambapo watu hawatili maanani, nafsi Yangu itatoweka. (Watu wa nyama na damu hawawezi kufikia hili, kwa hivyo ni vigumu kwenu kufikiri sasa.) Katika siku zijazo bado kutakuwa na jua, mwezi na mbingu na dunia ya asili, lakini kwa sababu nafsi Yangu itakuwa Sayuni, hakutakuwa na kuchomwa na jua au mchana na hakutakuwa kuteswa na maafa ya asili. Niliposema kuwa hatutahitaji taa au nuru ya jua kwa kuwa Mungu atatupa nuru, Nilikuwa nikizungumza juu ya kuwa Sayuni. Kulingana

na dhana ya wanadamu, kila kitu katika ulimwengu lazima kiondolewe na watu wote wanaishi katika mwanga Wangu. Wanafikiri hii ni maana halisi ya “hatutahitaji taa au nuru ya jua kwa sababu Mungu atatupa nuru,” lakini ni tafsiri isiyo sahihi ya hiyo. Niliposema “kila mwezi, mti ule utazaa aina kumi na mbili ya matunda,” Nilikuwa nikimaanisha mambo katika Sayuni. Sentensi hii inawakilisha kila kitu kuhusu maisha katika Sayuni. Katika Sayuni, wakati hautakuwa mdogo na hakutakuwa na upungufu wa jiografia wala nafasi. Ndiyo maana Nilisema “kila mwezi.” “Aina kumi na mbili ya matunda” haiwakilishi tabia unayodhihirisha unapoishi leo, inahusu maisha ya uhuru huko Sayuni. Maneno haya ni majumuisho ya maisha katika Sayuni. Kutoka kwa hili mtu anaweza kuona kwamba maisha katika Sayuni yatakuwa yenye fahari na yenye namna nyingi (kwa sababu hapa “kumi na mbili” inahusu ukamilifu). Yatakuwa maisha bila huzuni na machozi, hakutakuwa na unyonyaji au ukandamizaji hivyo wote watakombolewa na kuwa huru. Hii ni kwa sababu kila kitu kipo ndani ya nafsi Yangu, hakuna atakayevitenga, na kila kitu kitakuwa mandhari ya uzuri na upya wa milele. Utakuwa wakati ambapo kila kitu kitakuwa tayari, utakuwa mwanzo wa maisha yetu baada ya kurudi kwetu Sayuni.

Ingawa kazi Yangu duniani imekamilishwa kabisa, bado Nahitaji wazaliwa Wangu wa kwanza kufanya kazi duniani, hivyo Siwezi kurudi Sayuni bado. Siwezi kurudi Sayuni peke Yangu, Nataka kurudi Sayuni pamoja na wazaliwa Wangu wa kwanza baada ya wao kumaliza kazi yao duniani. Kwa njia hii, kunaweza kuitwa kupata utukufu kwa pamoja, hili litakuwa dhihirisho kamili la nafsi Yangu. (Nasema kuwa kazi ya wazaliwa Wangu wa kwanza duniani haijamalizwa bado kwa sababu wazaliwa Wangu wa kwanza bado hawajadhihirishwa. Kazi hii lazima ifanywe na watendaji huduma watiifu na waaminifu.)

Sura ya 116

Kati ya maneno Yangu, kunayo mengi ambayo huwafanya watu waogope. Maneno Yangu mengi huwafanya watu watetemeke kwa hofu, namaneno Yangu mengi huwafanya watu wateseke na kukata tamaa, na hata zaidi husababisha maangamizo ya watu. Hakuna anayeweza kuelewa wingi wa maneno Yangu au kuelewa wingi huo vizuri. Ni wakati Ninapowaambia maneno Yangu, sentensi kwa sentensi, na kuyafichua kwenu ndipo mnaweza kufahamu hali ya jumla ya mambo, huku mkisalia msiojua kuhusu sura kamili ya mambo mahsusi. Hivyo, Nitatumia ukweli kufichua maneno Yangu yote, na hapo kuwaruhusu mpate ufahamu wa juu zaidi. Tukizingatia mbinu ya usemi Wangu, sineni tu kwa maneno Yangu, lakini hata zaidi, Mimi natenda kwa maneno Yangu; hii ndiyo maana ya kweli ya “maneno na ufanikishaji kutendeka sawia.” Kwani na Mimi kila kitu ni bure, na kila kitu kinaachiliwa, na kwa msingi huu, yote Ninayoyafanya yamejazwa na hekima. Sineni kiholela, wala Sitendi kiholela. (Iwe ni

katika ubinadamu au uungu, Nanena na kutenda kwa hekima, kwa sababu ubinadamu Wangu ni sehemu isiyotenganika ya Mimi Mwenyewe.) Ilhali Ninaponena, hakuna anayezingatia sauti ya usemi Wangu; Ninapotenda, hakuna anayezingatia mbinu ya kazi Yangu. Huu ni upungufu wa mwanadamu. Nitafichua nguvu Yangu juu ya wanadamu wote, siyo tu juu ya wana wazaliwa Wangu wa kwanza, ila hata zaidi Nitafichua nguvu Yangu ndani ya mataifa yote na miongoni mwa watu wote; ni kufanya hivyo tu ndio ushuhuda wa nguvu unaomwaibisha Shetani. Sitendi kwa upumbavu. Watu wengi hufikiri kwamba ushuhuda Wangu kwa wana wazaliwa wa kwanza ni makosa; wanasema kwamba kuna Miungu wengine kando na Mimi, kwamba Natenda bila akili, kwamba Najishusha hadhi; na katika hili, upotovu wa mwanadamu unafunuliwa hata zaidi. Je, Naweza kuwa nimekosea katika kuwashuhudia wazaliwa wa kwanza? Mnasema kwamba Mimi nimekosea, basi, mnaweza kushuhudia? Isingelikuwa kwa sababu uinuaji Wangu, ushuhuda Wangu, bado mngemponda Mwana Wangu chini yenu, bado mngemtendea kwa kutojali kwa dharau, na bado mngemtendea kama mtumishi wenu. Ninyi kundi la nguruwe! Nitamtupa kila mmoja wenu kwa wakati wake! Hakuna atakayesamehewa! Niambieni, ni mambo ya aina gani ndiyo ambayo hayalingani na mtu aliye na ubinadamu wa kawaida? Bila shaka, wao ni nguruwe! Siwezi kuvumilia kabisa kuwaona. Ningesubiri ushuhuda wenu, kazi Yangu tayari ingekuwa imecheleweshwa! Ninyi kundi la nguruwe! Ninyi hamna ubinadamu kabisa hata kidogo! Sikuhitaji wewe unitumikie! Ondoka hapa wakati huu huu! Umemdhumu na kumnyanyasa Mwanangu kwa muda mrefu sana; Nitakukanyaga hadi upondekepondeke! Utaona kitakachofanyika ukithubutu kuwa mshenzi tena; utaona kitakachofanyika ukithubutu kuniaibisha tena! Tayari Nimekamilisha kazi Yangu kuu; Napaswa kugeuka na kuliangamiza kundi hili la wanyama!

Vyote vinakamilishwa mikononi Mwangu (Inavyohusiana na wale Ninaowapenda), na vyote pia vinaangamizwa mikononi Mwangu (kuhusiana na wale wanyama ambao Ninachukia, na wale watu, masuala na mambo Ninayodharau). Ninawaruhusu wazaliwa Wangu wa kwanza kuona yote Nitakayofanya, Ninawaruhusu waelewe kikamilifu na humo kuona yote ambayo Nimefanya tangu kutoka Sayuni. Baadaye, tutaingia pamoja katika Mlima Sayuni, kuingia mahali tulipokuwa kabla ya enzi, na kuishi maisha yetu upya. Kuanzia hapo kuendelea, hakutakuwa na mawasiliano zaidi na dunia na kundi hili la nguruwe, ila uhuru kamili; yote hayatazuiliwa na hayatakuwa na kizuizi. Ni nani anayethubutu kumkataa yeyote kati ya wazaliwa Wangu wa kwanza? Ni nani anayethubutu kuendelea kuwapinga wazaliwa Wangu wa kwanza? Sitamsamehe kwa urahisi! Bila kujali ulivyonicha hapo zamani, hivyo ndivyo lazima uwache wazaliwa Wangu wa kwanza leo. Usiwe namna moja mbele Yangu na nyingine nyuma Yangu; Mimi huona jinsi kila mtu alivyo kwa uwazi dhahiri. Kutokuwa mwaminifu kwa Mwana Wangu ni kutokuwa na upendo wa mtoto kwa mzazi Kwangu, ambao ni ukweli dhahiri, kwani

Sisi ni wa mwili mmoja. Ikiwa mtu ni mzuri Kwangu lakini ashikilie mtazamo tofauti kuelekea kwa wazaliwa Wangu wa kwanza, basi bila shaka ni uzao wa kawaida wa joka kuu jekundu, kwa sababu anauvunja mwili wa Kristo; dhambi hii haiwezi kusameheka kamwe! Kila mmoja wenu lazima aone hili. Ni wajibu wenu kunishuhudia, na zaidi ya hayo, ni wajibu wenu kuwashuhudia wazaliwa wa kwanza. Hakuna yeyote kati yenu atakayekwepa jukumu lake; Nitamtupa yeyote atakayevuruga mara moja! Usifikiri kwamba wewe ni kitu bora. Nakwambia sasa: Yeyote aliye hivyo sana, atakuwa mlengwa wa adhabu Yangu kali! Yeyote aliye hivyo ndiye aliye na tumaini la chini zaidi, na ndiye mwana wa kuangamia zaidi. Nitakuadibu milele!

Kazi Yangu yote inafanywa binafsi na Roho Wangu, na Siruhusu yeyote wa namna ya Shetani kuingilia. Hii ni ili kuepuka kuvuruga mipango Yangu. Mwishowe, Nitawaacha watu wazima na watoto wote wainuke na kunisifu na wazaliwa Wangu wa kwanza, wayasifu matendo Yangu ya ajabu, na kusifu udhihirisho wa nafsi Yangu. Nitaacha sauti ya sifa ingurume katika ulimwengu mzima na hadi miisho ya dunia, ikitikisa milima, mito, na vitu vyote, na Nitamwaibisha Shetani kikamilifu. Nitatumia ushuhuda Wangu kuharibu dunia nzima nzee chafu na ovu, na kutengeneza dunia mpya takatifu na safi. (Katika kusema jua, mwezi, nyota, na sayari za juu hazitabadilika baadaye, Simaanishi kwamba dunia nzee bado iko, ila kwamba dunia nzima itaharibiwa na dunia nzee itabadilishwa. Sinuii kuabadilisha ulimwengu.) Ni hapo tu ndipo itakuwa dunia inayolingana na mapenzi Yangu; ndani yake, hakutakuwa na aina hii ya uonevu iliyoko leo, wala hakutakuwa na hali ya sasa ya watu kunyanyasana. Badala yake, kutakuwa na usawa na busara kamili ndani ya mwili. (Ingawa Nasema kutakuwa na usawa na busara, itakuwa ndani ya mwili; itakuwa tofauti sana na ufalme Wangu—tofauti kama mbingu na dunia; hakuna njia ya kulinganisha hivyo viwili kabisa—hata hivyo, dunia ya binadamu ni dunia ya binadamu, na dunia ya roho ni dunia ya roho.) Wakati huo, wazaliwa Wangu wa kwanza na Mimi tutatumia mamlaka juu ya dunia kama hiyo (katika dunia hii hakutakuwa na vurugu kutoka kwa Shetani, kwa sababu Shetani atakuwa ametupwa nje kabisa na Mimi), lakini maisha yetu bado yatakuwa maisha ya ufalme, jambo ambalo hakuna mtu anayeweza kukana. Katika enzi zote, hakujawahi kuwa na binadamu yeyote (bila kujali jinsi alivyo mwaminifu) ambaye amepitia maisha ya aina hii, kwa sababu katika enzi zote, hakujawahi kuwa na mtu yeyote wa kuchukua wajibu wa mzaliwa Wangu wa kwanza, na bado atanitolea huduma baadaye. Ingawa hawa watendaji huduma ni waaminifu, wao hata hivyo ni uzao wa Shetani ambao wameshindwa na Mimi, hivyo baada ya kifo cha mwili bado wanazaliwa ndani ya dunia ya binadamu kufanya huduma kwa ajili Yangu; hii ndiyo maana ya kweli ya “wana hata hivyo ni wana, na watendaji huduma hata hivyo ni uzao wa Shetani.” Katika enzi zote haijulikani ni watu wangapi waliopo wa kufanya huduma kwa ajili ya wazaliwa wa kwanza wa leo; kati ya watendaji huduma wote, hakuna anayeweza kutoroka, na Nitawafanya wanitumikie milele. Kuhusiana na asili zao, wao wote ni wana wa

Shetani, na wote hunipinga Mimi, na ingawa wananifanyia huduma, wao hulazimishwa, na hakuna yeyote kati yao aliye na mbadala. Hii ni kwa sababu kila kitu kinadhibitiwa na mkono Wangu, na watendaji huduma Ninaowatumia lazima wanitumikie hadi mwisho. Hivyo, bado kuna watu wengi leo ambao wana asili sawa na manabii na mitume wa enzi zote, kwa sababu wao ni wa roho moja. Hivyo, bado kuna watendaji huduma wengi waaminifu ambao hukimbia huku na kule kwa ajili Yangu, lakini mwishowe (kwa miaka elfu sita, wamekuwa wakinifanyia huduma siku zote, kwa hivyo watu hawa ni miongoni mwa watendaji huduma), hakuna mtu anayeweza kupata kile ambacho wote katika enzi zote wamekitumainia, kwa sababu kile ambacho Nimetayarisha si kwa ajili yao.

Kila kitu Changu tayari kimekamilishwa mbele ya macho; Nitawafanya wazaliwa Wangu wa kwanza warudi nyumbani Kwangu na warudi upande Wangu, ili tuunganishwe. Kwa sababu Nimerudi kwa shangwe na ushindi na Nimepata utukufu kikamilifu, Naja kuwarudisha. Zamani, watu wengine walibashiri “mabikira watano wenye busara na mabikira watano wapumbavu”. Ingawa utabiri huo si sahihi, lakini pia si wenye makosa kabisa—hivyo, Naweza kuwapa ninyi maelezo fulani. “Mabikira watano wenye busara na mabikira watano wapumbavu” kwa pamoja hawawakilishi idadi ya watu wala aina ya mtu. “Mabikira watano wenye busara” inaashiria idadi ya watu, na “mabikira watano wapumbavu” inaashiria aina moja ya watu, lakini hakuna kati ya hivi viwili inayorejelea wana wazaliwa wa kwanza. Badala yake, vinawakilisha uumbaji. Hii ndiyo maana wameulizwa waandae mafuta katika siku za mwisho. (Viumbe hawana sifa Yangu; kama wanataka kuwa wale wenye busara, wanahitaji kuandaa mafuta, na hivyo wanahitaji kujitayarisha na maneno Yangu.) “Mabikira watano wenye busara” wanawakilisha wana Wangu na watu Wangu kati ya wanadamu Niliowaumba. Wanaitwa “mabikira” kwa sababu wanapatwa na Mimi, licha ya wao kuzaliwa duniani; mtu anaweza kuwaita watakatifu, kwa hivyo wanaitwa “mabikira.” “Watano” lililotajwa awali linawakilisha idadi ya wana Wangu na watu Wangu ambao Nimewajaalia. “Mabikira watano wapumbavu” linarejelea watendaji huduma, kwa kuwa wananifanyia huduma bila kushikilia hata umuhimu mdogo kwa maisha, wakifuatilia tu mambo ya nje (kwa sababu hawana sifa Yangu, bila kujali kile wanachokifanya, hicho ni kitu cha nje), na hawawezi kuwa wasaidizi Wangu wenye uwezo, kwa hiyo wanaitwa “mabikira wapumbavu.” “Watano” lililotajwa awali linamwakilisha Shetani, na ukweli kwamba wanaitwa “mabikira” kunamaanisha wameshindwa na Mimi na wanaweza kunifanyia Mimi huduma—lakini watu kama hao sio watakatifu, kwa hivyo wanaitwa watendaji huduma.

Sura ya 117

Wewe Ndiwe unayefungua kitabu, Wewe Ndiwe unayefungua mihuri saba, kwa sababu siri zote hutoka Kwako na baraka zote hufichuliwa na Wewe. Mimi sina budi kukupenda Wewe

milele, na Mimi sina budi kuwafanya watu wote wakuabudu Wewe, kwa sababu Wewe ni nafsi Yangu, Wewe ni sehemu ya onyesho Langu kamili lenye ukarimu, sehemu ya msingi ya mwili wangu. Kwa hiyo, ni lazima Mimi Nitoe ushahidi maalum. Ni nani mwingine kando na Yule mmoja aliye ndani ya nafsi Yangu anayefuata Moyo Wangu? Si Wewe Mwenyewe ambaye hutoa ushahidi kwa ajili Yako, lakini Roho Wangu ambaye hutoa ushahidi kwa ajili Yako, na kwa hakika Mimi sitamsamehe yeyote ambaye huthubutu kukupinga Wewe, kwa kuwa hili huhusu amri Zangu za utawala. Yote ambayo Wewe husema kwa hakika Nitayatimiza, na yote ambayo Wewe hufikiri kwa hakika Nitayakubali. Kama mtu fulani si mwaminifu kwako Wewe basi ananipinga Mimi kwa wazi, na kwa hakika Mimi Sitamsamehe. Mimi Nitawaadhibu kwa ukali wote ambao humpinga Mwanangu, na Mimi Nitawabariki wale ambao wanalingana na Wewe. Haya ndiyo mamlaka ambayo Mimi Ninakutunukia Wewe. Kwa yale yaliyosemwa zamani—matakwa na viwango vilivyowekwa kwa wana wa kiume wazaliwa wa kwanza—Wewe ni mfano mzuri. Hivyo ni kusema, vile Ulivyo ndiyo Nitakayohitaji kwa wazaliwa wa kwanza. Hiki si kitu ambacho binadamu wanaweza kufanya, lakini ni kile ambacho Roho Wangu Mwenyewe hufanya. Kama mtu yeyote huamini kuwa ni wanadamu ambao hushuhudia kwa ajili Yako basi kiumbe huyo bila shaka ni wa Shetani na adui Yangu! Kwa hiyo, shahidi ni mwenye kuondoa shaka, milele habadiliki, na kile ambacho Roho Mtakatifu huthibitisha! Hakuna yeyote anayeruhusiwa kubadilisha hilo kwa urahisi, na yeyote atakayefanya kitendo hicho, Mimi Sitasamehe! Kwa kuwa wanadamu hawawezi kuwa na ushuhuda kwa ajili Yangu, Mimi Mwenyewe hushuhudia kwa nafsi Yangu, na watu hawapaswi kuingilia kazi Yangu! Haya ni maneno ya hukumu kali ambayo kwayo kila mtu lazima awe mzingatifu!

Mnapaswa kufikiria na kuzingatia kila kitu katika yale Ninayoyasema Mimi. Usichukulie maneno Yangu kikawaida, bali sikiliza kwa makini. Kwa nini Mimi Ninasema kuwa wana wa kiume wazaliwa wa kwanza ni nafsi Yangu? Na sehemu ya msingi ya ufalme Wangu? Kabla ya enzi zote tuliishi pamoja na hatukuwahi kutengana kamwe. Kwa sababu ya mvurugo wa Shetani, baada ya Mimi kuwa mwili mara ya kwanza Mimi Nilirudi tena Sayuni. Kuendelea kutoka hapa, sisi sote tulikuja katika dunia, na baada ya Mimi kupata ushindi katika siku za mwisho—yaani, baada ya mimi kuwapata nyinyi tena kutoka kwa mwili ambao Shetani amepotosha—Mimi nitawaleta tena Sayuni ili nafsi Yangu iweze kuungana tena, kutotenganishwa tena kamwe. Baada ya hayo Mimi Sitapata mwili upya tena, na nyinyi hakika hamtatoka katika mwili Wangu. Hiyo ni kusema, baada ya hapo Mimi Sitaiumba dunia tena, lakini Nitabaki milele bila kutenganishwa na wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza katika Sayuni, kwa sababu kila kitu kimekamilishwa kwelikweli, na Mimi Nimekaribia kuhitimisha enzi nzee nzima. Ni katika Sayuni tu ambako kuna maisha ya mbingu na nchi mpya, kwa kuwa nafsi Yangu hupatikana Sayuni. Hakutakuwa na mbingu mpya au dunia mpya zaidi ambazo zipo bali na hii. Mimi ni

mbingu mpya, na Mimi pia ni nchi mpya, kwa sababu nafsi Yangu hujaza Sayuni nzima. Pia inaweza kusemwa kwamba wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza ni mbingu mpya, wana Wangu wa kiume wazaliwa wa kwanza ni nchi mpya. Wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza na Mimi ni wa mwili mmoja, wa kutotenganishwa. Kusema juu Yangu ni lazima kujumuishe wana wa kiume wazaliwa wa kwanza, na Mimi hakika Sitamsamehe yeyote ambaye hujaribu kututenganisha. Wakati Ninayafanya mataifa yote na watu kurejea mbele ya kiti Changu cha enzi, mashetani yote yatafedhehiwa na mapepo machafu yatatoroka kwa woga mbali na Mimi. Halafu ni hakika kuwa haki itakuwepo miongoni mwa watu wote (kumaanisha miongoni mwa wana Wangu wa kiume na watu), na ni hakika kuwa hakutakuwa na vurugu zozote za Shetani katika mataifa yote, kwa maana Mimi Nitakuwa Nikishikilia uongozi juu ya ulimwengu dunia wote na watu wa mataifa, na mashetani yatakuwa yameharibiwa kwelikweli, kushindwa kabisa, na watakuwa wakipokea adhabu ya amri Zangu za utawala.

Mimi Ninaendelea na kazi miongoni mwa watu wote, lakini wao wana nuru ya Roho Wangu tu, na hakuna hata mmoja kati yao mwenye sifa zinazostahili kufunua mafumbo Yangu, hakuna yeyote mwenye sifa zinazostahili kunionyesha Mimi. Ni Yule tu mtu ambaye huja kutoka Kwangu tu mwenye sifa zinazostahili za kufanya kazi Yangu, jinsi ilivyo kwa wengine, Mimi huwatumia tu watu hao kwa muda. Roho Wangu hatamshukia mtu kiholela, kwa kuwa kila kitu ndani Yangu ni cha thamani. Kwa Roho Wangu kushuka juu ya mtu fulani na kwa Roho Wangu kufanya kazi kwa mtu fulani ni vitu tofauti kabisa. Roho Wangu hufanya kazi kwa watu walio nje Yangu, lakini Roho Wangu hushuka juu ya Yule mtu ambaye hutoka Kwangu. Haya ni mambo mawili yasiyohusiana kabisa. Kwa vile mtu Huyo atokaye Kwangu ni mtakatifu, lakini wale walio nje Yangu si watakatifu, bila kujali ni wazuri kiasi gani wanaweza kuwa. Roho Wangu hatamshukia mtu kwa sababu yoyote ndogo. Watu hawapaswi kuwa na wasiwasi. Mimi huwa Sifanyi makosa yoyote, na Mimi ni asilimia mia moja kwa uhakika kuhusu Ninayofanya! Kama ambavyo Nimemshuhudia Yeye, kwa hakika Nitamlinda Yeye pia; Mtu huyo waziwazi hutoka Kwangu na ni sehemu ya msingi ya nafsi Yangu. Kwa hiyo, Natumaini watu wanatenga dhana zao wenyewe, waache mawazo waliyopewa na Shetani, waamini kila tamko Langu kuwa ni la kweli, na hawayaruhusu mashaka kuingia katika mawazo yao. Hili ndilo Agizo Langu kwa binadamu, ushawishi Wangu kwa binadamu. Kila mtu lazima ayashike mambo haya, kila mtu lazima kwa kweli ayatii, na ni lazima ayachukue Ninayoyasema Mimi kuwa ndicho kiwango.

Mimi sipaswi tu kuanza kazi Yangu kati ya mataifa yote na watu wote tu, lakini pia Mimi kuanza kazi Yangu kila mahali katika ulimwengu dunia, na hii inaonyesha hata zaidi kuwa siku ya kurudi Kwangu Sayuni haiko mbali sana (kwa sababu ni muhimu Kwangu kurudi Sayuni kabla Niweze kuanza kazi kati ya watu wote na kote katika ulimwengu dunia). Je, kuna mtu yeyote ambaye anaweza kuzielewa hatua za kazi Yangu na njia ambayo Mimi hufanya kazi? Sababu ya

Mimi kusema Nitakutana na wageni katika roho ni kwa sababu hili kimsingi haliwezi kufanyika katika mwili, na kwa sababu Mimi sitaki kubahatisha hatari kwa mara ya pili. Hizi ndizo sababu za kuwasiliana kwa karibu na wageni katika roho. Hii itakuwa katika dunia ya kweli ya kiroho, siyo dunia fulani ya kiroho isiyo dhahiri kama inavyowazwa na wale^[a] wanaoishi katika mwili. Kile Ninachokisema wakati huo kitakuwa ni tofauti tu katika jinsi Mimi husema kwani itakuwa ni enzi tofauti. Kwa hiyo, Mimi Nawakumbusha binadamu tena na tena kuhakiki jinsi ambavyo Mimi hunena, na Mimi Nawakumbusha wanadamu pia kwamba kuna siri katika kile ambacho Mimi husema ambacho watu hawawezi kukifunua. Lakini hakuna anayeelewa kwa nini Mimi Nasema vitu hivi, na kwa sababu tu Mimi Nawaambia hili leo ndipo muweze kuelewa kidogo, lakini bado si kabisa. Baada ya enzi hii katika kazi Yangu, Mimi nitawaarifu hatua kwa hatua. (Bado Mimi Ninataka kuondoa baadhi ya watu kupitia hili, hivyo Mimi Sitasema chochote kwa sasa.) Hii ndiyo njia ya hatua ifuatayo katika kazi Yangu. Kila mtu anapaswa kuhakiki na kuona wazi kwamba Mimi ni Mungu Mwenyewe ambaye ni wa busara.

Tanbihi:

a. Maandiko ya awali hayana maneno “kama inavyowazwa na wale.”

Sura ya 118

Yeyote atakayeinuka kumshuhudia Mwana Wangu, Nitampa neema; yeyote ambaye hatainuka kumshuhudia Mwana Wangu, ila badala yake apinge na kutumia dhana za mwanadamu ili Amtathmini, Nitamwangamiza. Lazima wote waone waziwazi! Kumshuhudia Mwana Wangu ni kitendo cha kunicha nako kunayaridhisha mapenzi Yangu. Usimheshimu tu Baba lakini umdhulumu na kumkandamiza Mwana. Wale wanaofanya hivyo ni wa dhuria ya joka kuu jekundu na Sihitaji watu duni kama hawa kumshuhudia Mwanangu; Nitawaangamiza katika shimo lisilo na mwisho. Nawataka watendaji huduma waaminifu na wa kweli kutoa huduma kwa Mwanangu, na Simhitaji yeyote kati ya wengine wote. Hii ni tabia Yangu ya haki na inatumika kuonyesha kwamba Mimi ni Mungu Mwenyewe mtakatifu na Asiye na dosari. Sitamsamehe yeyote anayezikosea amri Zangu za utawala. Yeyote aliyekuasi au kukutesa zamani, iwe katika familia au dunia, Nitamwadibu mmoja mmoja na hakuna atakayehurumiwa, kwani hakuna sehemu Yangu ambayo ni ya mwili na damu. Kutoa ushuhuda ka ajili Yako leo kunaonyesha kwamba wale watendaji huduma wamemaliza kutoa huduma kwa ajili Yangu, hivyo usiwe na haya yoyote na usiwe na mashaka. Wao ni watendaji huduma Wako hata hivyo na hatimaye Wewe ni wa mbinguni, na Utarudi kwa mwili Wangu mwishowe, kwani mwili Wangu hauwezi kuwa bila Wewe. Wale waliokuasi na ambao hawakulingana na Wewe zamani (hili ni jambo ambalo wengine hawawezi kuliona, ila Wewe pekee Unalijua moyoni mwako) sasa wamefichua maumbo yao ya asili na wameanguka, kwani Wewe ni Mungu Mwenyewe na

Hutavumilia yeyote kukuasi au kukukosea. Ingawa haiwezi kuonekana hata kidogo kutoka nje, Roho Wangu yuko ndani Yako na hili ni dhahiri. Lazima watu wote waliamini, fimbo Yangu ya chuma isije ikawaua wale wote wanaoniasi! Kwa sababu Ninakushuhudia, hakika Unabeba mamlaka, na kila kitu Unachosema ni maonyesho Yangu, kila kitu Unachokifanya ni dhihirisho Langu, kwani Wewe ni mpendwa Wangu na Wewe ni sehemu ambayo nafsi Yangu haiwezi kuwa bila. Hivyo kila kitendo Chako, kile Unachovaa, kile Unachotumia, na mahali Unapoishi—hakika pia ni matendo Yangu. Hakuna anayepaswa kujaribu kutafuta kitu dhidi Yako, na hakuna anayepaswa kukutia makosani. Iwapo yeyote atafanya hili, Sitamsamehe!

Nitawatoa watumishi wote waovu kutoka kwa nyumba Yangu, na ndani ya nyumba Yangu Nitawafanya watumishi wote waaminifu wawashuhudie wazaliwa Wangu wa kwanza; huu ndio mpango Wangu na ni jinsi ambayo Ninafanya kazi. Wakati watumishi waovu wanapomshuhudia Mwana Wangu inanuka kama wafu nami Ninaichukia. Wakati watumishi Wangu waaminifu wanapomshuhudia Mwana Wangu ni kwa ari na uaminifu, na inakubalika Kwangu. Hivyo, yeyote asiye tayari kumshuhudia Mwana Wangu, ondoka hapa sasa hivi! Sitakulazimisha. Nikikuambia uondoke basi lazima uondoke! Angalia matokeo kwako ni yapi na kile kinachokusubiri, na wale wanaotoa huduma wanaelewa hili zaidi kuliko mtu mwingine yeyote. Hukumu Yangu, hasira Yangu, laana Zangu, kuchoma Kwangu na ghadhabu Yangu kali na yenye hasira vitawafika wowote wanaoniasi wakati wowote. Mkono Wangu haumwonyeshi yeyote huruma; bila kujali jinsi yule anayehudumia alivyokuwa mwaminifu awali, akimwasi Mwana Wangu leo basi Nitamwangamiza mara moja na Sitamweka mbele Yangu. Kutokana na hili mtu anaweza kuuona mkono Wangu usio na huruma. Kwa sababu watu hawanijui na asili zao zinaniasi, hata wale walio waaminifu Kwangu ni kwa ajili ya raha yao wenyewe. Iwapo jambo litatokea la kuwaathiri vibaya, mioyo yao inabadilika mara moja na wanataka kukimbia kutoka upande Wangu. Hii ndiyo asili ya Shetani. Hampaswi kuwa wanaoshikilia maoni yenu, mkijiamini kuwa waaminifu! Kama hakuna manufaa kwao, kundi hili la wanyama hawawezi kuwa waaminifu Kwangu kabisa. Nisingetangaza amri Zangu za utawala, mngekuwa mlikimbia zamani. Nyote sasa mko matatani, msitake kunihudumia lakini msitake kuangushwa kwa mkono Wangu. Nisingetangaza kwamba maafa makuu yatawafika wowote wanaoniasi wakati wowote, mngekuwa mngekimbia kitambo. Je, Sijui ujanja ambao watu wanaweza kuugeukia? Watu wengi zaidi sasa wanahodhi matumaini haba, lakini matumaini hayo yanapogeuka na kuwa masikitiko hawataki kuendelea zaidi na wanaomba kurudi. Nimekwisha kusema awali kwamba Simweki yeyote hapa kinyume cha mapenzi yake, lakini tahadhari kufikiria matokeo yatakavyokuwa kwako, ni huu ni ukweli, si Mimi kukutisha wewe. Hakuna awezaye kuielewa asili ya mwanadamu isipokuwa Mimi, na wote wanafikiria kwamba wao ni watiifu Kwangu, pasipo kujua kwamba utiifu wao ni mchafu. Uchafu huu utawaangamiza watu kwa kuwa wao ni

njama ya joka kubwa jekundu. Hilo lilidhihirishwa na Mimi zamani sana; Mimi ni mwenyezi Mungu, na je, Mimi singeweza kufahamu jambo rahisi kama hili? Mimi ninaweza kupenyeza damu yako na mwili wako ili kuziona nia zako. Si vigumu Kwangu kuielewa asili ya mwanadamu, lakini watu hujaribu kuwa wajuaji, wakifikiria kwamba hakuna mtu ajuaye nia zao isipokuwa wao wenyewe. Je, hawajui kwamba, mwenyezi Mungu anaishi ndani ya mbingu na dunia na vitu vyote?

Nitampenda Mwana Wangu hadi mwisho kabisa na Nitalichukia joka kuu jekundu pamoja na Shetani milele hata milele. Kuadibu Kwangu kutawajia wale wote wanaoniasi na hakuna adui hata mmoja atakayehurumiwa. Nimesema awali, “Naweka jiwe kubwa Sayuni. Kwa waumini, jiwe hili ni msingi wa ujenzi wao. Kwa wale wasioamini, hili ni jabali linalowakwaza. Kwa wana wa ibilisi, hili ni jiwe linalowaponda hadi wafe.” Sijasema maneno haya awali tu, ila yametabiriwa na watu wengi na watu wengi wameyasoma katika enzi hii. Aidha, watu wengine wamejaribu kueleza maneno haya, lakini hakuna mtu amewahi kufumbua siri hii awali, kwa sababu kazi hii inafanywa tu wakati uliopo wa siku za mwisho. Hivyo, ingawa watu wengine wamejaribu kuyaeleza maneno haya maelezo yao yote ni uongo. Leo, Nafichua maana nzima kwenu ili mweze kujua uzito wa Mimi kuwashuhudia wazaliwa Wangu wa kwanza, na kusudi Langu katika kufanya hivyo. Naweka jiwe kubwa Sayuni na jiwe hili linarejelea wazaliwa Wangu wa kwanza wakishuhudiwa. Neno “kubwa” halimaanishi kwamba kushuhudia huku kunafanywa kwa kiwango fulani kikubwa kabisa, ila badala yake kwamba katika kuwashuhudia wazaliwa Wangu wa kwanza, watendaji huduma wengi zaidi watakimbia. Hapa, “wale wasioamini” wanarejelea wale wanaokimbia kwa sababu Mwana Wangu anashuhudiwa, kwa hiyo jiwe ni kipingamizi kwa mtu wa ina hii. Nasema ni jabali kwa sababu mtu wa aina hii atauawa kwa mkono Wangu, kwa hiyo jabali linalowasababisha watu kujikwaa halisemwi kuhusiana na kuanguka au kuwa dhaifu, ila linasemwa kuhusiana na kuuawa kwa mkono Wangu. “Waumini” katika “Kwa waumini, jiwe hili ni msingi wa ujenzi wao” wanarejelea wale watendaji huduma ambao ni waaminifu, na “msingi wa ujenzi wao” unarejelea neema na baraka ambazo watapokea baada ya wao kunihudumia kwa uaminifu. Kwamba wazaliwa wa kwanza wameshuhudiwa inaonyesha kwamba enzi hii yote nzee itapita punde, na inaashiria uharibifu wa ufalme wa Shetani; kwa hiyo, kwa mataifa ni jabali linalowaponda hadi wafe. Hivyo kuyavunjavunja mataifa yote na kuwa vipande vipande inarejelea dunia nzima kufanywa upya kabisa; mambo ya zamani yatapita na mapya yataanzishwa—hii ndiyo maana ya kweli ya “kuvunjavunja.” Je, mnaelewa? Kazi Ninayoifanya katika hatua hii ya mwisho inaweza kufupishwa kwa maneno haya machache tu. Hili ni tendo Langu la ajabu na unapaswa kuyaelewa mapenzi Yangu ndani ya maneno Yangu.

Sura ya 119

Ni lazima nyote muelewe nia Zangu, nyote mnapaswa kuelewa hali Yangu ya moyo. Sasa ni wakati wa kujiandaa kurudi Sayuni, sina mawazo ya lolote isipokuwa hili. Mimi Ninatumaini tu kwamba Ninaweza kukutana nanyi siku moja hivi karibuni, na kutumia kila dakika na kila sekunde pamoja nanyi katika Sayuni. Mimi Naichukia kabisa dunia, Nauchukia kabisa mwili, na Mimi Namchukia kabisa hata zaidi kila binadamu duniani; Sina nia ya kuwaona, kwa sababu wote ni kama mapepo, bila hata chembe ya asili ya binadamu; Sina nia ya kuishi duniani, Mimi Nawachukia kabisa viumbe wote, Mimi Nawachukia kabisa wote ambao ni wa mwili na damu. Nchi yote inavunda maiti; Mimi Nataka kurudi Sayuni mara moja, ili kuiondoa harufu yote mbaya ya maiti kutoka dunia, na kufanya dunia yote ijae sifa kwa ajili Yangu. Mimi Nitarejea Sayuni, Mimi Nitajiondoa kutoka kwa mwili na ulimwengu, hakuna yeyote anayepaswa kuweka kizuizi mbele Yangu; Mkono wangu ambao huua mwanadamu hauna hata chembe ya hisia! Kuanzia sasa na kuendelea, hakuna yeyote anayepaswa kunena juu ya ujenzi wa kanisa, vinginevyo Mimi sitamsamehe. (Hii ni kwa sababu sasa ni wakati wa kushuhudia wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza, wakati wa kujenga ufalme; yeyote anenaye juu ya ujenzi wa kanisa anaubomoa ujenzi wa ufalme na kuukatiza usimamizi Wangu.) Lote liko tayari, lote limetayarishwa, lote libakilo ni kwa wana wazaliwa wa kiume wa kwanza kutukuzwa, kushuhudiwa, na wakati hayo yanapofanyika Mimi, bila kuchelewa kwa muda na bila kuzingatia mtindo, lazima Nirudi Sayuni mara moja—mahali mnapashikilia mawazoni mwenu usiku na mchana. Msiangalie tu jinsi dunia ilivyo laini na thabiti sasa; lakini kazi hii yote ni kuhusu hali ya kurudi Sayuni; msijali kuhusu mambo hayo sasa, na wakati siku ya kurudi Sayuni inapowadia yote yatakuwa kamili. Ni nani asiyetaka kurudi Sayuni hivi punde? Ni nani asiyetaka Baba na wana wa kiume kupatana hivi karibuni? Bila kujali jinsi anasa za duniani zinavyofurahisha, haziwezi kuweka mshiko juu ya miili yetu; tutavuka mipaka ya miili yetu na kwa pamoja kurudi Sayuni. Ni nani huthubutu kuzuia? Ni nani huthubutu kuweka vikwazo? Mimi bila ya shaka Sitamsamehe! Mimi Nitaviondoa vikwazo vyote. (Sababu Ninasema siwezi kurejea Sayuni mara moja ni kwa sababu ya hili. Mimi Natekeleza kazi hii ya utakasaji sawia na Ninavyoshuhudia wanangu wazaliwa wa kiume wa kwanza; kazi hizi mbili zinaendelea kwa wakati mmoja. Kazi ya utakasaji inapokamilika, utakuwa ni wakati wa Mimi kuwafichua wana wa kiume wazaliwa wa kwanza. Vikwazo ambavyo Nimezungumzia vinarejelea idadi kubwa ya watenda huduma, hivyo Ninasema kwamba kazi hizi mbili zinafanyika sawia.) Nitawafanya wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza wazunguke pamoja na Mimi kote ulimwenguni na kufika miisho ya dunia, kuvuka milima na mito na vitu vyote; ni nani huthubutu kukwamisha? Ni nani huthubutu kuzuia? Mkono Wangu haumuachilii kwa urahisi mtu yeyote; mbali na wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza, Mimi hughadhibika dhidi ya na kuwalaani wote. Kuvuka nchi nzima hakuna mwenye

kufa hata mmoja ambaye hupata baraka Zangu; wote hukumbana na laana Yangu. Tangu mwanzo wa uumbaji wa dunia, Mimi Sijambariki yeyote; hata wakati Mimi Nimepeana baraka imekuwa maneno tu, haijawahi kamwe kuwa uhalisi, kwa sababu Mimi Ninamchukia Shetani kwa hali ya juu, na Mimi Sitawahi kamwe kumbariki, ila kumwadhibu tu. Ni mwishowe tu, baada ya Mimi kumshinda Shetani kikamilifu, baada ya ushindi kamili kuwa Wangu, Nitakapowapa baraka za yakinifu wahudumu wote waaminifu, Niwaache wanisifu Mimi kama starehe, kwa sababu kazi Yangu itakuwa imekamilika.

Kwa kweli muda Wangu hautakuwa mrefu zaidi, mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita unafikia ukamilisho mbele ya macho yako. (Hakika ni mbele ya macho yako; siyo kuonyesha kabla, unaweza kuona kutoka kwa hali Yangu ya moyo.) Mimi Nitawachukua wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza mara moja hadi nyumbani Sayuni. Baadhi ya watu watasema, “Kwa kuwa ni kwa ajili ya wazaliwa wa kwanza tu, kwa nini Utumie miaka elfu sita yenye thamani ya wakati? Na kwa nini Ufanye watu wengi?” Nimesema kabla kuwa kila kitu Changu ni cha thamani. Ni jinsi gani wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza wasiwe hivyo hata zaidi? Mimi Nitawahamasisha wote kunitumikia Mimi, na zaidi ya hayo, Mimi Nitafichua nguvu Yangu, ili kila mtu aweze kuona kwamba katika ulimwengu dunia wote hakuna kitu hata kimoja ambacho hakimo mikononi mwetu, hakuna mtu hata mmoja ambaye hayuko katika huduma Yetu, na hakuna ufanikishaji hata mmoja ambao haujatekelezwa kwa ajili yetu. Mimi nitafanikisha kila kitu. Kwangu Mimi hakuna wazo la muda; ingawa Mimi nadhamiria kuukamilisha mpango na kuikamilisha kazi Yangu kwa miaka elfu sita, kwangu Mimi yote yamekombolewa na huru. Hata kama ni chini ya miaka elfu sita, mradi kwa maoni Yangu wakati umefika, ni nani angethubutu kutamka neno la upinzani? Ni nani angethubutu kusimama na kuhukumu apendavyo? Kazi Yangu, Mimi hufanya Mwenyewe; Muda wangu, Mimi hupanga Mwenyewe. Hakuna mtu, hakuna jambo, hakuna kitu huthubutu kutenda kimakusudi; Mimi nitavifanya vyote vinifuata. Kwangu Mimi hakuna jema au bovu; Mimi Nikisema ni jema, ni jema kabisa; Mimi Nikisema ni bovu, hilo ni kweli pia. Hupaswi daima kutumia dhana za binadamu kunipima Mimi! Mimi Ninasema wana wa kiume wazaliwa wa kwanza pamoja na Mimi tumebarikiwa—ni nani huthubutu kukataa kunyenyekea? Mimi Nitakuangamiza papo hapo! Wakataa kunyenyekea! Wewe ni muasi! Mimi sina huruma kabisa kwa ajili ya wanadamu wote, Mimi nimewachukia kwa kiasi fulani; Mimi siwezi kabisa kuwa mvumilivu zaidi. Kulingana na Mimi, ulimwengu dunia wote ni lazima uangamizwe mara moja, ni hapo tu ndipo kazi Yangu kubwa itakapokamilishwa, ni hapo tu ndipo usimamizi wa mpango Wangu wa usimamizi utakapokamilishwa, ni hapo tu ndipo chuki iliyo moyoni Mwangu itakapoondoka. Sasa Mimi Ninajali tu kuhusu kushuhudia wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza, masuala mengine yote Mimi Nitayaweka kando na kutojali kwa sasa; kwanza fanya jambo lililo kuu, kisha fanya jambo

la kufuata. Hizi ndizo hatua za kazi Yangu, hakuna yeyote anayepaswa kuenda kinyume na hili, wote lazima wafuate Ninayosema Mimi, ili wasiwe malengo ya laana Yangu.

Sasa kazi yangu imekamilishwa, Mimi Ninaweza kupumzika. Kuanzia sasa na kuendelea, Mimi Sitafanya kazi tena, Mimi Nitawaambia wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza wafanye yote ambayo Mimi Ninataka yafanywe kwa ajili Yangu, kwa sababu wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza ni Mimi, wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza ni nafsi Yangu; hivi si vibaya hata kidogo; msifuate dhana na kuhukumu. Kuwaona wana wa kiume wazaliwa wa kwanza ni kuniona Mimi, kwa sababu sisi ni kitu kimoja; yeyote ambaye hututenganisha sisi kwa hivyo ananipinga Mimi, na Mimi sitamsamehe. Kwa maneno Yangu, kuna mafumbo yasiyoeleweka kwa mwanadamu. Wale tu Ninaowapenda Mimi wanaoweza kunionyesha Mimi, na hakuna wengine wanaoweza kulifanya; hili huamuliwa na Mimi, na hakuna anayeweza kulibadilisha. Maneno Yangu ni ya thamani, maneno Yangu ni yenye maarifa na ya kina kirefu. Wote ni lazima watumie juhudi kubwa kwa maneno Yangu, jaribuni kuyatafakari maneno Yangu mara kwa mara, msikose neno hata moja au sentensi, vinginevyo watachukua maana yenye makosa, na kutoyaelewa maneno Yangu. Mimi Nimesema tabia Yangu haivumilii kosa, ikimaanisha kuwa wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza walioshuhudiwa hawawezi kupingwa. Wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza huwakilisha kila kipengele cha tabia Yangu, kwa hivyo tarumbeta takatifu inapopigwa, hapo ndipo Mimi Ninapoanza kuwashuhudia wana wa kiume wazaliwa wa kwanza; na hivyo baadaye tarumbeta takatifu itakuja baadaye kuwa tangazo taratibu la tabia Yangu kwa halaiki. Kwa maneno mengine, wakati wana wa kiume wazaliwa wa kwanza wanapofichuliwa, huo ndio utakuwa wakati ampapo tabia Yangu inafichuliwa. Ni nani anayeweza kulielewa hili? Mimi nasema hayo hata katika mafumbo niliyoyafichua Mimi, hapo yanabaki mafumbo ambayo watu hawawezi kufumbua. Ni nani kati yenu ambaye kwa kweli amejaribu kuelewa maana ya kweli ya maneno haya? Tabia Yangu ni nafsi ya mtu kama vile ambavyo mmefikiria? Ni kosa la kijinga lililoje! Leo yeyote ambaye huona wanangu wa kiume wazaliwa wa kwanza ni kitu cha baraka na huona tabia Yangu, hili ni kweli kabisa. Wanangu wazaliwa wa kwanza huniwakilisha Mimi mzima, bila shaka yoyote ni nafsi Yangu. Hakuna yeyote anayepaswa kutilia hili shaka! Walio watiifu wanabarikiwa na neema, na waasi wanalaaniwa. Hili ndilo Ninaloamrisha Mimi, na hakuna yeyote anayeweza kulibadilisha!

Sura ya 120

Sayuni! Salamu! Sayuni! Ita kwa sauti! Nimerudi kwa ushindi, Nimerudi nikiwa mshindi! Watu wote! Harakisheni mpange foleni kwa utaratibu! Vitu vyote! Mtakuja kusimama kabisa, kwa sababu nafsi Yangu inaukabili ulimwengu mzima na nafsi Yangu inaonekana katika

Mashariki ya dunia! Nani anayethubutu kutopiga magoti katika ibada? Nani anayethubutu kutoniita Mungu wa kweli? Nani anayethubutu kutoangalia juu kwa kumcha? Nani anayethubutu kutotoa sifa? Nani anayethubutu kutangaza kwa shangwe? Watu wangu wataisikia sauti Yangu, Wanangu watasalia ndani ya ufalme Wangu! Milima, mito, na vitu vyote vitashangilia bila kukoma, na kurukaruka bila kupumzika. Wakati huu, hakuna atakayethubutu kurudi nyuma, hakuna atakayethubutu kusimama katika upinzani. Hili ni tendo Langu la ajabu, na hata zaidi ni nguvu Yangu kuu! Nitafanya kila kitu kiniche Mimi katika moyo wake na hata zaidi Nitafanya kila kinisifu Mimi. Hili ni lengo la msingi la mpango Wangu wa usimamizi wa miaka elfu sita, nami Nimeamua hili. Hakuna hata mtu mmoja, hakuna hata kitu kimoja wala jambo moja, linathubutu kusimama kunipinga Mimi, au linathubutu kusimama kushindana na Mimi. Watu wangu wote wataelekea mlimani Kwangu (hili linaonyesha dunia ambayo Nitaiumba baadaye) nao watatii mbele Zangu kwa sababu Ninao uadhama na hukumu, nami Nina mamlaka. (Hili linahusu wakati Niko katika mwili. Pia Ninayo mamlaka katika mwili lakini kwa sababu upungufu wa muda na nafasi hayawezi kuzidi kiwango katika mwili, kwa hiyo haiwezi kusemwa kwamba Nimepata utukufu kamili. Ingawa Nawapata wazaliwa wa kwanza katika mwili, bado haiwezi kusemwa kwamba Nimepata utukufu. Ni wakati tu Nitakaporudi Sayuni na kubadilisha sura Yangu ndipo inaweza kusemwa kwamba Nina mamlaka, yaani, Nimepata utukufu.) Hakuna kitu kitakuwa kigumu Kwangu. Kila kitu kitaharibiwa kwa maneno kutoka kinywani Mwangu, na ni kwa sababu ya maneno kutoka kinywani Mwangu ndipo yatatukia na kufanyika kamili, hiyo ni nguvu Yangu kuu na hayo ni mamlaka Yangu. Kwa sababu Nina nguvu tele na nimejawa na mamlaka, hakuna mtu anayeweza kuthubutu kunizuia Mimi. Tayari Nimepata ushindi juu ya kila kitu na Nimewashinda wana wote wa uasi. Nawaleta wazaliwa Wangu wa kwanza pamoja kurudi Sayuni. Si Mimi pekee Yangu Ninayerejea Sayuni. Kwa sababu hii wote watawaona wazaliwa Wangu wa kwanza na hivyo watakuza moyo wa uchaji kwa ajili Yangu. Hili ni lengo Langu katika kuwapata wazaliwa Wangu wa kwanza na umekuwa mpango Wangu tangu wakati Wangu wa kuiumba dunia.

Wakati kila kitu kiko sawa, hiyo ndiyo siku ambayo Nitarudi Sayuni, na siku hii itakumbukwa na watu wote. Nitakaporudi Sayuni, vitu vyote duniani vitakuwa kimya na vitu vyote duniani vitakuwa na amani. Wakati ambapo Nimerudi Sayuni, kila kitu kitarejelea sura yake ya awali. Wakati huo, Nitaianza kazi Yangu katika Sayuni, Nitawaadhibu waovu na kuwatuza wazuri, Nitaleta mamlakani haki Yangu nami Nitatekeleza hukumu yangu. Nitatumia maneno Yangu kukamilisha kila kitu na kumfanya kila mtu na kila kitu kipitie mkono Wangu unaoadibu. Nitawafanya watu wote wauone utukufu Wangu mzima, waione hekima Yangu nzima, wauone ukarimu Wangu mzima. Hakuna mtu yeyote atathubutu kusimama kutoa hukumu kwani yote imekamilika nami. Katika hili, kila mtu ataiona heshima Yangu yote na wote

watapata uzoefu wa ushindi Wangu wote kwa kuwa kila kitu kimewekwa wazi nami. Kutokana na haya, mtu anaweza kuuona uwezo Wangu mkubwa vizuri, na kuyaona mamlaka Yangu. Hakuna mtu atathubutu kunikosea Mimi, hakuna mtu atathubutu kunizuia Mimi. Yote yamewekwa waziwazi nami, nani angethubutu kuficha kitu chochote? Nina uhakika wa kutomwonyesha huruma! Mafidhuli mno kama wao lazima waipokee adhabu Yangu kali na watu wabaya kabisa kama wao lazima waondolewe kutoka machoni Pangu. Nitawatawala kwa fimbo ya chuma nami Nitayatumia mamlaka Yangu kuwahukumu, bila huruma yoyote na bila kutowaudhi kabisa, kwa maana Mimi ni Mungu Mwenyewe Nisiye na hisia na ambaye ni mwadhimu na Siwezi kukosewa. Hii inapaswa kueleweka na wote na kuonekana na wote ili kuepuka “bila kusudi au sababu” kuangushwa nami, kuangamizwa nami, wakati utakapofika, kwa kuwa fimbo Yangu itawaangusha wote ambao wananikosea. Sitajali kama wanajua amri Zangu za utawala au la; hilo halitakuwa muhimu Kwangu kwa kuwa nafsi Yangu haiwezi kuvumilia kosa la mtu yeyote. Hii ndiyo sababu imesemwa kwamba Mimi ni simba; yeyote Ninayemgusa, Nitawaangusha. Hii ndiyo sababu inasemwa kuwa sasa kusema kwamba Mimi ni Mungu wa huruma na wema ni kunikufuru. Kwa asili Mimi si Mwanakondoo bali ni simba. Hakuna mtu anayethubutu kunikosea na yeyote anayenikosea Nitamwadhibu mara moja kwa kifo, bila hisia hata kidogo! Kutokana na hili, mtu anaweza kuiona tabia Yangu vizuri. Kwa hiyo, katika enzi ya mwisho kundi kubwa la watu likijitoa, hilo ni jambo ambalo ni gumu kwa wanadamu kuvumilia, lakini Nina raha na furaha na sioni hii kama kazi ngumu hata kidogo, hiyo ni tabia Yangu.

Natarajia kwamba watu wote watakuwa na moyo mtiifu ili kufuata yote yanayotokana na Mimi. Kwa njia hiyo, bila shaka Nitawabariki wanadamu sana kwa sababu Nimesema kwamba wale ambao wanalingana nami watahifadhiwa huku wale ambao ni maadui Kwangu wataalaaniwa. Nimeamua hili na hakuna yeyote anaweza kulibadilisha. Mambo hayo ambayo Nimeamua ni mambo ambayo Nimekamilisha na yeyote atakayekwenda kinyume nayo ataadibiwa mara moja. Nina kila kitu ninachohitaji Sayuni na kila kitu ambacho Nina hamu nacho. Hakuna dalili ya dunia Sayuni na ukilinganishwa na dunia ni kasri tajiri na kuu, lakini hakuna mtu ameingia ndani yake na hivyo haipo kabisa katika mawazo ya mwanadamu. Maisha Sayuni ni tofauti na maisha duniani; duniani, maisha ni kula, kuvaa, kucheza, na kutafuta furaha, ilhali Sayuni ni tofauti sana. Ni maisha ya Baba na wana waliozama katika furaha, wakijijaza daima nafasi yote ya ulimwengu, lakini kila mara pia wakija pamoja kwa umoja. Kwa kuwa sasa mambo yamefika katika kiwango hiki leo, Nitawaambia mahali ambapo Sayuni uko. Sayuni uko Ninapoishi, ni eneo la nafsi Yangu. Kwa hiyo, lazima Sayuni uwe mahali patakatifu, na ni lazima iwe mbali sana na dunia. Kwa hiyo, Nasema kwamba Ninawadharau watu, vitu na masuala ya dunia, Ninachukia sana kula, kunywa, kucheza na kutafuta raha kwa mwili, kwa

sababu bila kujali jinsi anasa za dunia zinavyofurahisha, haziwezi kulinganishwa na maisha katika Sayuni; ni tofauti kati ya mbingu na dunia na hakuna njia ya kulinganisha hizi mbili. Sababu ambayo kuna mafumbo mengi ambayo mwanadamu hawezi kufumbua duniani yote ni kwa sababu watu hawajasikia chochote kuhusu Sayuni. Naam, Sayuni uko wapi hata hivyo? Je, iko katika anga za juu kama watu wanavyoifikiria kuwa? Hapana! Hayo ni mawazo tu katika akili za wanadamu. Mbingu ya tatu ambayo Nimeitaja inafikiriwa na watu kuwa na maana ya ishara, lakini ufahamu uliodhaniwa katika akili za wanadamu ni kinyume kabisa cha maana Yangu. Mbingu ya tatu ambayo Ninanena kuihusu hapa si uongo hata kidogo. Hii ndiyo sababu Nasema kwamba Sitaviharibu jua, mwezi, nyota, na miili ya mbinguni, nami Sitaziondoa mbingu na dunia. Je, Naweza kuharibu makazi Yangu? Naweza kuuondoa Mlima Sayuni? Je, hili si jambo la kuchekesha? Mbingu ya tatu ni makazi Yangu, ni Mlima Sayuni, na jambo hili ni hakika. (Kwa nini Nasema kwamba hii ni halisi? Ni kwa sababu Ninachosema sasa hakiwezi kueleweka kabisa na mwanadamu, anaweza tu kukisikia. Upeo wa kufikiri wa mwanadamu hauwezi kukijumuisha kabisa, na kwa hiyo Nitasema tu kiasi hiki kuhusu Sayuni ili kuwaepusha watu kuiona kama hadithi tu.)

Baada Yangu kurudi Sayuni, wale walio duniani wataendelea kunisifu Mimi kama zamani. Wale watendaji huduma waaminifu wanabaki wakisubiri kutoa huduma Kwangu lakini kazi yao itakuwa imefika mwisho. Jambo bora zaidi wanaloweza kufanya ni kutafakari hali Yangu kuwa duniani. Wakati huo, Nitaanza kushusha maafa juu ya wale ambao watakabiliwa na maafa makubwa; ilhali kila mtu anaamini kwamba Mimi ni Mungu mwenye haki. Bila shaka Sitawaadhibu wale watendaji-huduma waaminifu, bali nitawaruhusu tu wapokee neema Yangu. Maana Nimesema kuwa nitawaadhibu watenda dhambi wote, na kwamba wale wanaotekeleza matendo mema watapata starehe yakinifu iliyokirimiwa nami, huu ni ufunuo kwamba Mimi ni Mungu wa haki na uaminifu Mwenyewe. Nitakaporudi Sayuni, Nitaanza kugeuka kuelekea kila taifa duniani; Nitawaleta Waisraeli kwa wokovu na kuwaadibu Wamisri. Hii ni hatua inayofuata katika kazi Yangu. Kazi Yangu wakati huo haitakuwa sawa kama siku hizi: Haitakuwa kazi katika mwili lakini itauzidi mwili kabisa, na kwa kuwa Nimenena, itafanyika, na kama Nilivyoagiza, itasimama imara. Mradi imesemwa nami, itatimizwa mara moja katika hali halisi, na hii ndiyo maana ya kweli ya neno Langu kunenwa na kutimizwa kwake kufanyika kwa wakati mmoja, kwa sababu Ninachosema ni mamlaka yenyewe. Sasa Ninanena kuhusu baadhi ya mambo ya jumla ili kuwasaidia watu duniani kuwa na dalili chache bali si kufahamu ovyo ovyo. Wakati huo utakapofika, kila kitu kitapangwa nami na hakuna anayepaswa kutenda kimakusudi ili kuepuka kuangushwa kwa mkono Wangu. Katika mawazo ya wanadamu, yote Ninenayo si dhahiri, kwa sababu hata hivyo namna ya mwanadamu ya kufikiri ni finyu, na mawazo ya mwanadamu na yale ambayo Nimesema yako mbali sana kama mbingu na ardhi. Kwa hiyo,

hakuna anayeweza kuyafumbua na jambo bora zaidi ni kukubaliana na kile Ninachosema, huu ni mwelekeo usiobadilika wala kuzuilika. Nimesema: “Katika siku za mwisho, mnyama ataibuka kuwatesa watu Wangu na wale ambao wanaogopa kifo watawekewa alama na muhuri ili kunyakuliwa na mnyama. Wale ambao wameniona watauawa na mnyama.” “Mnyama” katika maneno haya bila shaka inarejelea Shetani ambaye huwadanganya watu, hiyo ni kusema kwamba Nitakaporudi Sayuni, kundi kubwa la watendaji huduma litajiondoa, yaani, litanyakuliwa na mnyama. Viumbe hawa wote watarudi katika shimo lisilo na mwisho kupokea kuadibu Kwangu kwa milele. “Wale ambao wameniona” inaashiria wale watendaji huduma waaminifu ambao wameshindwa nami. “Baada ya kuniona” inamaanisha wao kushindwa nami. “Kuuawa na mnyama” inahusu Shetani, kushindwa na Mimi, asithubutu kusimama kunipinga Mimi, hiyo ni kusema, Shetani hatathubutu kufanya kazi yoyote juu ya watendaji huduma hawa. Kwa hiyo, nafsi za watu hawa zitakuwa zimehifadhiwa, na hii inachangia uwezo wao wa kuwa waaminifu Kwangu, ambayo ni kusema kwamba wale watendaji huduma waaminifu watakuwa na uwezo wa kuipokea neema Yangu na baraka Yangu. Kwa hiyo, Nasema kwamba nafsi zao zitakuwa zimeokolewa (hii haimaanishi kupaa hadi mbingu ya tatu, ambayo ni dhana tu ya mwanadamu). Lakini wale watumishi wabaya watafungwa tena na Shetani na kisha watatupwa katika shimo lisilo na mwisho. Hii ni adhabu Yangu kwao, ni adhabu kwa ajili yao, na ni kile ambacho makosa yao yanastahili.

Kufuatia kuharakisha hatua kwa kazi Yangu, wakati Wangu duniani unapungua hatua kwa hatua. Tarehe ya kurudi Kwangu Sayuni yanakaribia. Wakati ambapo kazi Yangu duniani imefika mwisho, utakuwa wakati wa kurudi Kwangu Sayuni. Sipendi kuishi duniani kamwe, lakini kwa ajili ya usimamizi Wangu, kwa ajili ya mpango Wangu, Nimevumilia mateso yote. Leo, wakati umekwishafika. Nitaharakisha hatua Zangu, na hakuna mtu anayeweza kuenda kwa mwendo sawa nami. Kama watu wanaweza kulielewa au la, Nitawaambia kwa kina yote ambayo mwanadamu hawezi kuelewa lakini wale kati yenu mlio duniani mnahitaji kujua. Kwa hiyo, Nasema kwamba Mimi ni Mungu Mwenyewe Ninayeushinda wakati na nafasi. Isingekuwa ili kuwapata wazaliwa wa kwanza na hivyo kumshinda Shetani, Ningekuwa tayari nimerudi Sayuni, au hasa nisingekuwa Nimewaumba wanadamu. Ninaudharau ulimwengu wa mwanadamu, Nawachukia sana watu walio mbali nami, hata kufikia kiwango cha kufikiria kuwaangamiza wanadamu wote kwa dharuba moja. Hata hivyo, kazi Yangu inayo utaratibu na muundo, ina kadiri na kiasi, haiko bila taratibu. Yote ambayo Ninafanya ni ili kumshinda Shetani, na hata zaidi ili Niweze kuwa pamoja na wazaliwa Wangu wa kwanza haraka iwezekanavyo. Hili ni Lengo langu.

Sehemu ya Pili

Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima (Februari 20, 1992 hadi Juni 1, 1992)

Utangulizi

“Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima” ni sehemu ya pili ya matamshi yaliyoonyeshwa na Kristo. Ndani ya sehemu hii, Kristo Anatumia utambulisho wa Mungu Mwenyewe. Yanajumlisha kipindi cha kuanzia Februari 20, 1992 hadi Juni 1, 1992, na yana jumla ya sura arobaini na saba. Namna, maudhui na mtazamo wa maneno ya Mungu katika matamshi haya hayafanani kabisa na “Matamko ya Kristo Mwanzoni.” “Matamko ya Kristo Mwanzoni” inafichua na kuongoza tabia ya watu ya nje na maisha yao rahisi ya roho. Hatimaye, inaisha kwa “majaribu ya watendaji huduma.” Hata hivyo, “Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima,” inaanza na hitimisho la utambulisho wa watu kama watendaji huduma na mwanzo wa maisha yao kama watu wa Mungu. Inaongoza watu ndani ya kipeo cha pili cha kazi ya Mungu, ambapo katika mkondo wake wanapitia majaribu ya jahanamu, majaribu ya kifo, na nyakati za kumpenda Mungu. Hatua hizi kadhaa zinafichua kikamilifu ubaya wa mwanadamu mbele ya Mungu na tabia yake ya kweli. Hatimaye, Mungu anamaliza na sura ambapo Anatengana na mwanadamu, hivyo kukamilisha hatua zote za kupata mwili huku kwa ushindi wa Mungu wa kikundi cha kwanza cha watu.

Katika “Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima,” Mungu anaonyesha maneno Yake kutoka kwa mtazamo wa Roho. Namna ambavyo Anazungumza haiwezi kufikiwa na wanadamu walioumbwa. Aidha, msamiati na mtindo wa maneno Yake ni mzuri na wa kuisimua, na hakuna mtindo wowote wa maandishi ya binadamu ungechukua nafasi yake. Maneno ambayo Anatumia kumfichua mwanadamu ni sahihi, ni yasiokanushika na falsafa yoyote, nayo huwafanya watu wote kutii. Kama upanga wenye ncha kali, maneno Anayotumia kumhukumu mwanadamu hukata moja kwa moja hadi kwa kina cha nafsi za watu, hata kuwaacha bila mahali pa kujificha. Maneno Anayotumia kuwafariji watu yana huruma na wema wenye upendo, ni kunjufu kama kumbatio la mama mwenye upendo, na huwafanya watu wahisi salama kuliko walivyowahi hapo awali. Sifa moja kubwa zaidi ya matamshi haya ni kwamba, wakati wa hatua hii, Mungu hazungumzi kwa kutumia utambulisho wa Yehova au Yesu Kristo, wala wa Kristo wa siku za mwisho. Badala yake, kwa kutumia utambulisho Wake wa asili—Muumba—Anazungumza kwa na kuwafunza wote wanaomfuata Yeye na ambao bado hawajamfuata Yeye. Ni haki kusema kwamba hii ilikuwa mara ya kwanza tangu uumbaji kwa Mungu kuwahutubia wanadamu wote. Mungu hakuwa amewahi kuzungumza kwa wanadamu walioumbwa kinaganaga hivyo na kwa utaratibu sana. Bila shaka, hiyo pia ilikuwa mara ya kwanza Alipozungumza mengi hivyo, na kwa muda mrefu sana, kwa wanadamu wote. Ilikuwa ya kipekee kabisa. Na zaidi, matamshi

haya yalikuwa maneno halisi ya kwanza yaliyoonyeshwa na Mungu miongoni mwa wanadamu ambapo Aliwafichua watu, akawaongoza, akawahukumu, na kuzungumza nao wazi wazi na kwa hiyo, pia, yalikuwa matamshi ya kwanza ambayo kwayo Mungu aliwaruhusu watu wajue nyayo Zake, mahali Anapokaa, tabia ya Mungu, kile Mungu anacho na alichio, mawazo ya Mungu, na sikitiko Lake kwa wanadamu. Inaweza kusemwa kwamba haya yalikuwa matamshi ya kwanza ambayo Mungu alikuwa amezungumza kwa wanadamu kutoka mbingu ya tatu tangu uumbaji, na mara ya kwanza ambapo Mungu alikuwa ametumia utambulisho Wake wa asili kuonekana na kuonyesha sauti Yake kwa wanadamu katikati ya maneno.

Matamshi haya ni ya kina na magumu sana; si rahisi kuyaelewa, wala haiwezekani kufahamu asili na makusudi ya maneno ya Mungu. Hivyo, Kristo ameongeza ufafanuzi baada ya kila sura, kwa kutumia lugha iliyo rahisi kwa mwanadamu kufahamu kuleta uwazi kwa sehemu kubwa zaidi ya matamshi hayo. Hili, likiunganishwa na matamshi yenyewe, linayafanya kuwa rahisi sana kwa kila mtu kuyaelewa na kuyajua maneno ya Mungu. Tumeyafanya maneno haya kiambatisho kwa “Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima.” Ndani yake, Kristo anatoa ufafanuzi kwa kutumia maneno yaliyo rahisi sana kuelewa. Uunganishaji wa hayo mawili ni uoanishaji kamili wa uungu na Mungu katika ubinadamu. Ingawa Mungu anazungumza katika mtazamo wa nafsi ya tatu katika kiambatisho, hakuna anayeweza kukana kwamba maneno haya yalitamkwa na Mungu binafsi, kwani hakuna binadamu anayeweza kuyafafanua maneno ya Mungu kwa dhahiri; ni Mungu Mwenyewe pekee anayeweza kufafanua asili na makusudi ya matamshi Yake. Hivyo, ingawa Mungu huzungumza kwa kutumia njia nyingi, makusudi ya kazi Yake hayabadiliki kamwe, wala lengo la mpango Wake haligeuki kamwe.

Ingawa “Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima” inamalizika kwa sura ambayo ndani yake Mungu anatengana na mwanadamu, kwa kweli, huu ndio wakati ambapo kazi ya Mungu ya ushindi na wokovu miongoni mwa mwanadamu, na kazi Yake ya kuwafanya watu wakamilifu, ilionyeshwa kwa mara ya kwanza rasmi. Hivyo, inafaa zaidi kwetu kuchukulia “Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima” kama unabii wa kazi ya Mungu ya siku za mwisho. Kwani ni baada ya wakati huu tu ndipo Mwana wa Adamu aliyepata mwili alianza rasmi kufanya kazi na kuzungumza kwa kutumia utambulisho wa Kristo, akitembea miongoni mwa makanisa na kutoa uzima, na kunyunyizia na kuwachunga watu Wake wote—ambako kulisababisha matamshi mengi katika “Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani.”

Sura ya 1

Je, wale wanaoshuhudia maneno Yangu huyakubali kwa kweli? Je, mnanijua kwa kweli? Mmejifunza utiifu kweli? Ninyi hutumia rasilimali kwa ajili Yangu kwa uaminifu? Mmekuwa na ushuhuda thabiti, usiokubali kushindwa Kwangu mlipokabiliwa na joka kuu jekundu? Je, moyo

wenu wa ibada hulifedhehesha kweli joka kuu jekundu? Ni kupitia tu kwa jaribio la maneno Yangu ndipo Naweza kutimiza lengo Langu la kulitakasa kanisa na kuwachagua wale wanaonipenda Mimi kweli. Nisingetenda kwa njia hii, kuna yeyote angenijua Mimi? Ni nani angeweza kujua uadhama Wangu, ghadhabu Yangu, na hekima Yangu kupitia kwa maneno Yangu? Nitakamilisha Nilichoanza, lakini bado ni Mimi nipimaye mioyo ya wanadamu. Kwa kweli, hakuna mwanadamu anayenielewa Mimi kwa ukamilifu, kwa hiyo Ninamwongoza kwa maneno, na kumwongoza katika mwongo mpya kwa njia hii. Mwishowe Nitatumia maneno kukamilisha kazi Yangu yote, Nikiwafanya wale wote wanaonipenda kwa dhati kurudi kwa ufalme Wangu kwa utiifu, kuishi mbele ya kiti Changu cha enzi. Hali sio kama ilivyokuwa wakati fulani, na kazi Yangu imeingia katika kiwango kipya cha kuanza. Hilo likiwa hivyo, kutakuwa na njia mpya: Wale wanaolisoma neno Langu na kulikubali kama uzima wao kabisa ndio watu wa ufalme Wangu. Kwa vile wako katika ufalme Wangu, wao ni watu Wangu katika ufalme. Kwa sababu wanaongozwa na maneno Yangu, ingawa wanatajwa kama watu Wangu, jina hili si la chini ya kuitwa “wana” Wangu. Baada ya kufanywa kuwa watu wa Mungu, wote ni lazima wawe waaminifu katika ufalme Wangu na kutimiza majukumu yao, na wale wanaokosea amri Zangu za usimamizi lazima wapate adhabu Yangu. Hili ni onyo Langu kwa wote.

Kwa sasa njia mpya inatumika, yale yote kutoka wakati uliopita hayahitaji kusemwa tena. Hata hivyo, Nimeyasema maneno haya: Kile Nilichosema lazima kihesabiwe, kile kilichohesabiwa lazima kikamilishwe, na hili haliwezi kubadilishwa na yeyote; hili ni thabiti. Kama ni kile Nilichosema katika wakati uliopita au Nitakachosema katika siku za usoni, yote yatatimia, na wanadamu wote wataliona hili. Hii ni kanuni inayoelekeza maneno na kazi Yangu. Tangu ujenzi wa kanisa tayari umetimizwa, sasa sio tena enzi ya ujenzi wa kanisa, lakini badala yake ni enzi ambayo kwayo ufalme unajengwa kwa ufanisi. Hata hivyo, kwa vile bado mko duniani, makusanyiko yenu yatabaki kujulikana kama “kanisa.” Hata hivyo, kiini cha kanisa sio kama kilivyokuwa wakati fulani, na kimeonyesha ufanisi wa kweli. Kwa hivyo, Nasema kwamba ufalme Wangu umeshuka duniani. Hakuna anayeweza kuelewa kiini cha maneno Yangu, wala hawezi kufahamu kusudi la maneno hayo. Ninapozungumza leo, mnaweza kupitia epifania. Labda wengine wataangua kilio; baadhi huenda wakahisi woga kwamba hivi ndivyo Mimi huzungumza. Baadhi huenda wakashikilia maoni ya mtindo wa zamani wanapotazama kila hatua Yangu; baadhi huenda wakajuta kwa baada ya kueleza malalamiko yao au kunipinga Mimi wakati ule. Kwangu; wengine huenda wakafurahia kimoyomoyo, kwani hawajawahi kupotea kutoka kwa jina Langu, na sasa leo wamehuishwa; labda watu wengine waliochacharishwa na maneno Yangu zamani sana, na wanakaribia kifo, wamevunjika moyo na ni wenye huzuni, hawana tena moyo wa kuyasikia maneno Niyazungumzayo, hata Nikichagua njia tofauti ya kueleza. Huenda kuna wengine ambao wamejitolea sana Kwangu hata hawajawahi kulalamika,

wasioshuku kamwe, leo wana bahati sana kupata kufunguliwa na kuhisi shukrani isiyoelezeka ndani ya mioyo yao Kwangu. Hali hizi zote zilizotajwa zinaweza kutumika kwa viwango tofauti tofauti, kwa kila binadamu. Lakini kama vile wakati uliopita ni wakati uliopita, na sasa ni wakati uliopo, hakuna haja ya kutamani tena wakati uliopita, au kuwa na wasiwasi kuhusu siku za usoni. Miongoni mwa wanadamu, wale wanaoenda kinyume cha uhalisi na hawafanyi mambo kulingana na uongozi Wangu hawatakuwa na mwisho mzuri, na watajiletea tu matatizo. Kwa kila kitu kinachotokea ulimwenguni, hakuna kitu Nisichokuwa na usemi wa mwisho kukihusu. Ni kitu gani kilichopo ambacho hakiko mikononi Mwangu? Chochote Nisemacho hufanyika, na miongoni mwa wanadamu, ni nani aliyepo anayeweza kuyabadilisha mawazo Yangu? Yaweza kuwa agano Nililofanya juu ya dunia? Hakuna chochote kinachoweza kuuzuia mpango Wangu; Mimi huwepo wakati wote katika kazi Yangu na vilevile katika mpango wa usimamizi Wangu. Ni mwanadamu gani anaweza kuingilia? Je, sio Mimi binafsi Niliyetengeneza mipango hii? Kuingia katika hali hii leo, bado haipotei kutoka kwa mpango Wangu au Nilichoona mbele; yote iliamuliwa Nami zamani sana. Ni nani miongoni mwenu anaweza kufahamu mpango Wangu wa hatua hii? Watu Wangu wataisikiliza sauti Yangu, na kila mmoja wa wale wanaonipenda kwa kweli atarudi mbele ya kiti Changu cha enzi.

Februari 20, 1992

Sura ya 2

Kufuata kuanza kazi kwa mtazamo mpya, kutakuwa na hatua mpya katika kazi Yangu. Kama ilivyo katika ufalme, Nitafanya mambo moja kwa moja kupitia kwa uungu, Nikiongoza kila hatua ya njia, sahihi hadi kwa maelezo madogo, na bila kutiwa najisi na nia za binadamu hata kidogo. Yafuatayo yanaeleza kwa muhtasari namna ya utekelezaji halisi: Kwa vile ni kupitia katika ugumu na usafishaji ndiyo wamepata jina la “watu”, na kama walivyo watu wa ufalme Wangu, lazima Niwafanye watii kwa mahitaji kali, ambayo ni ya juu kushinda mbinu za kazi Yangu kwa vizazi vilivyopita. Huu sio tu uhalisi wa maneno, bali pia la muhimu zaidi ni uhalisi wa kutenda, na hili lazima kwanza litimizwe. Katika kila neno na matendo, ni lazima watosheleze viwango vinachohitajika kwa watu wa ufalme, na mkosaji yeyote ataondolewa mara moja, ili kuzuia aibu kulijia jina Langu. Hata hivyo, wale wasiojua ambao hawawezi kuona kwa dhahiri, na hawawezi kuelewa ni wa kipekee. Katika ujenzi wa ufalme Wangu, tilia maanani kula na kunywa maneno Nisemayo, uielewe hekima Yangu, na kuthibitisha kupitia kazi Yangu. Yeyote anayetilia maanani maneno ya kitabu kisicho Changu hahitajiki na Mimi kabisa; huyu ni kahaba anayeniasi. Kama mtume, mtu hapaswi kuishi nyumbani kwa muda mrefu. Kama hili haliwezi kufanyika, Nitamtupilia mbali na Sitamtumia tena. Simlazimishi. Kwa kuwa mitume hawako nyumbani kwa muda mrefu, ni kwa kushinda kanisani kwa muda mrefu ndiyo

wanarekebisha maadili. Kwa kila mikusanyiko miwili ya kanisa, mitume wanapaswa kuhudhuria angalau mara moja. Kwa hivyo, mikutano ya wafanyikazi wenza lazima ikuwe ya kawaida (mikutano ya wafanyakazi wenza inajumuisha: mikusanyiko yote ya mitume, mikusanyiko yote ya wakuu wa kanisa, na mikusanyiko yote ya watakatifu walio na utambuzi ulio wazi). Angalau wengine wenu mtaweza lazima wahudhurie kila mkusanyiko, na mitume wanatilia maanani tu kuchunga makanisa. Mahitaji yaliyowekwa awali kwa watakatifu yamekuwa ya undani zaidi. Kwa wale waliotenda makosa kabla Nilishuhudie jina Langu, kwa ajili ya kujitoa kwao Kwangu, bado Nitawatumia baada ya wao kujaribiwa na Mimi. Hata hivyo, kwa wale wanaotenda kosa tena baada ya ushuhuda Wangu na wanakusudia wa kuanza ukurasa mpya wa maisha yao, watu kama hao hubaki tu ndani ya kanisa. Bado, hawawezi kuwa wavivu na watukutu, badala yake wawe wanaojizua zaidi ya wengine. Na kwa wale wasiorekebisha mienendo yao baada ya Mimi kunena sauti Yangu, Roho Wangu atawaacha mara moja, na kanisa litakuwa na haki ya kutekeleza hukumu Yangu, na kuwafanya kutoka kanisani. Hili ni bila shaka, na hakuwezi kuwa na nafasi zaidi ya kufikiria. Mmoja akizirai katika majaribu, yaani, akiondoka, hakuna mtu anapaswa kujishughulisha na mtu huyo, ili kuepuka kunijaribu Mimi na kumruhusu Shetani kuingia kanisani kwa wendawazimu. Hii ndiyo hukumu Yangu kwake. Yeyote anayetenda udhalimu na kutenda kulingana na hisia zake mwenyewe pia hatahesabiwa miongoni mwa watu Wangu, sio tu yule aliyeasi. Kazi nyingine ya mitume ni kulenga kuisambaza injili. Bila shaka, watakatifu pia wanaweza kufanya kazi hii, lakini lazima wawe wenye hekima katika kufanya hivyo, na pia lazima wajizue kutokana na kuamsha shida. Yaliyotajwa hapa juu ndiyo mbinu ya sasa ya kutenda. Pia tena kama kumbusho, unafaa kuweka maanani kufanya mahubiri yako kuwa yenye undani zaidi, ili kwamba wote waweze kuingia katika ukweli wa maneno Yangu. Lazima uyafuate maneno Yangu kwa ukaribu na kuyafanya yawe kwamba watu wote wapate kuyaelewa vizuri, na bila utata. Hili ni la muhimu sana. Wale kati ya watu Wangu wanaohodhi mawazo ya usaliti lazima waondolewe, na wasiruhusiwe kukaa katika nyumba Yangu kwa muda mrefu, wasije wakaleta tusi kwa jina Langu.

Februari 21,1992

Sura ya 3

Kwa kuwa mnaitwa watu Wangu, mambo hayapo kama yalivyokuwa; mnapaswa kusikiliza na kutii matamshi ya Roho Wangu, fuateni kwa karibu kazi Yangu, na msitenganishe Roho Wangu na mwili Wangu, maana kwa asili Sisi ni wamoja, na Hatujatengana. Yeyote ambaye angegawanya Roho na mwanadamu na kuzingatia kwa mwanadamu au Roho atapata hasara na ataweza tu kunywa kutoka kwenye kikombe chake chungu—ni hayo tu. Ni wale tu ambao wanaweza kumtazama Roho na mwanadamu kama kitu kizima kisichoweza kutenganishwa ndio

wataweza kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu Mimi, na ni hapo tu ndipo mabadiliko yanaweza kutokea taratibu katika maisha yaliyomo ndani yao. Ili kwamba hatua inayofuata ya kazi Yangu iweze kuendelea taratibu na bila kizuizi, Ninatumia usafishaji wa maneno kuwajaribu wale wote ambao wapo katika nyumba Yangu, Nikitumia mbinu ya kufanya kazi kuwajaribu wale ambao hunifuata Mimi. Katika mazingira haya, ni haki kusema kwamba wote wanapoteza matumaini; kama watu, hakuna mmoja miongoni mwao ambaye hali zake si hasi na za baridi, kana kwamba nafasi yao yote imebadilika. Baadhi ya watu wanaishutumu Mbingu na nchi; baadhi, katika kukata tamaa kwao, bado wanastahimili ugumu na kukubali jaribio la maneno Yangu; baadhi wanatazama angani na kushusha pumzi ndefu, machozi yanajaza macho yao, kana kwamba wanahangaikia kifo cha mapema mno cha mtoto mchanga aliyezaliwa; baadhi hata wanahisi kuna aibu katika kuishi hivyo, na wanamwomba Mungu awachukue karibuni; baadhi wanashinda siku nzima wakiwa wamepigwa bumbuwazi, kana kwamba wamekuwa wagonjwa sana na bado hawajarejea katika hali yao ya kawaida; baadhi, baada ya kulalamika, wanaondoka kimyakimya; na baadhi bado hunisifu Mimi kutoka mahali pao, lakini wao bado ni hasi kidogo. Leo, ambapo yote yamefichuliwa, Sihadhi kuzungumzia zaidi yaliyopita; jambo la muhimu mkubwa ni kwamba mnapaswa bado muwe na uwezo wa utiifu mkubwa sana kutoka kwa mahali Ninayowapa leo, ili kwamba yote mnayofanya yakidhi idhini Yangu, na yote msemayo ni zao la mwangaza na nuru Yangu, na hatimaye kile mnachoishi kwa kudhihirisha ni sura Yangu, ni udhihirisho Wangu kabisa.

Maneno Yangu yanatolewa na kuonyeshwa wakati wowote au mahali popote, na hivyo, nyinyi pia, mnapaswa kujijua wenyewe mbele Yangu wakati wote. Kwani leo ni, hata hivyo, tofauti na kile kilichokuja kabla, na hamwezi tena kutimiza chochote mnachotamani. Badala yake, kwa kuongozwa na maneno Yangu, mnapaswa kuweza kuihini miili yenu, mnapaswa kutumia maneno Yangu kama nguzo, na hampaswi kutenda kizembe. Njia zote kuelekea matendo ya kweli kwa ajili ya kanisa zinaweza kupatikana katika maneno Yangu. Wale ambao hawatendi kulingana na maneno Yangu wanakosea Roho Wangu moja kwa moja, na Nitawaangamiza. Kwa kuwa mambo yamefikia hali ilivyo leo, hamhitaji kujihihi kutiwa uchungu na kujuta kuhusu matendo yenu ya zamani. Ukarimu Wangu hauna mipaka kama ilivyo bahari na anga—uwezo na ufahamu wa mwanadamu kunihusu Mimi unawezaje kukosa kujulikana Kwangu kama kiganja Changu? Ni nani miongoni mwa wanadamu ambaye hayupo mikononi Mwangu? Unadhani Sijui chochote juu ya jinsi ukubwa wa kimo chako ulivyo unaamini Mimi sijui kabisa kuhusu hili? Hilo haliwezekani! Hivyo, wakati ambapo watu wote wapo katika hali yao ya kukata tama zaidi, wakati ambapo hawawezi kusubiri zaidi, na wanatamani kuanza upya, wakati wanapotaka kuniuliza nini kinaendelea, wakati ambapo baadhi wanajiendekeza katika ubadhirifu na baadhi wanataka kuasi, wakati baadhi bado ni watiifu

wakifanya huduma, Ninaanza sehemu ya pili ya enzi ya hukumu: kuwatakasa na kuwahukumu watu Wangu. Ambayo ni kusema, Ninaanza rasmi kuwafundisha watu Wangu, kuwawezesha si tu kunitolea ushuhuda unaopendeza, bali, zaidi, kutimiza ushindi mzuri katika vita kwa ajili Yangu kutoka kwa kiti cha watu Wangu.

Nyakati zote, watu Wangu wanapaswa kujihadhari dhidi ya hila danganyifu za Shetani, walinde lango la nyumba Yangu kwa ajili Yangu, waweze kusaidiana na kupeana mahitaji, kitu ambacho kitawazuia kuingia katika mtego wa Shetani, wakati mtakapokuwa na majuto ya kuchelewa sana. Kwa nini Ninawafundisha kwa hali hiyo ya dharura? Kwa nini Ninawaelezea ukweli wa ulimwengu wa kiroho? Kwa nini Ninawakumbusha na kuwaonya mara kwa mara? Je, mmewahi kufikiri juu ya hili? Je, mmewahi kulielewa? Hivyo, hamhitaji tu kuweza kuwa wazoefu kwa kutegemeza juu ya msingi wa zamani, bali, zaidi, kuondoa uchafu ndani yenu chini ya uongozi wa maneno ya leo, mkiruhusu kila maneno Yangu kukita mzizi na kustawi ndani ya roho zenu, na muhimu zaidi, kuzaa matunda zaidi. Hiyo ni kwa sababu kile Ninachokiomba si maua angavu yaliyostawi sana, bali matunda mengi—matunda, zaidi ya hayo, ambayo hayaharibiki. Je, mnaelewa maana ya kweli ya maneno Yangu? Ingawa maua katika nyumba ya kioo ya kuhifadhi mimea ni yasiyohesabika kama nyota, na huwavuta watalii wote, mara yanaponyauka yanakuwa mabovu mabovu kama hila danganyifu za Shetani, na hakuna mtu anayevutiwa nayo. Lakini kwa wale ambao wamerushwa na upepo na kuchomwa na jua na kuwa na ushuhuda Kwangu, ingawa maua haya si mazuri, mara yanaponyauka, hapo panatokea tunda, maana haya ndiyo matakwa Yangu. Ninapozungumza maneno haya, mnaelewa kiwango kipi? Mara maua yanaponyauka na kuzaa matunda, na mara matunda haya yote yanaweza kutolewa kwa ajili ya furaha Yangu, Nitakamilisha kazi Yangu yote duniani, na Nitaanza kufurahia udhihirisho wa hekima Yangu!

Februari 22, 1992

Sura ya 4

Watu Wangu wote wanaohudumu mbele Zangu wanapaswa kutafakari kuhusu siku zilizopita: Je, upendo wenu Kwangu ulikuwa umetiwa doa na uchafu? Je, uaminifu wenu Kwangu ulikuwa safi na wa moyo wako wote? Je, ufahamu wenu kunihusu ulikuwa wa kweli? Je, Nilikuwa na nafasi kiasi gani katika nyoyo zenu? Je, Nilikuwa Nimejaza nyoyo zenu zote? Je, maneno Yangu yalitimiza kiasi gani ndani yenu? Msinichukue kama mpumbavu! Hivi vitu viko wazi kabisa Kwangu! Leo, sauti ya wokovu Wangu inapopazwa nje, je, kumekuwa na ongezeko la upendo wenu Kwangu? Je, sehemu ya uaminifu wenu Kwangu imekuwa safi? Je, ufahamu wenu kunihusu umezidishwa? Je, sifa ya zamani iliweka msingi dhabiti kwa maarifa yenu leo

hii? Je, ni kiasi gani cha undani wenu kinamilikiwa na Roho Wangu? Mfano Wangu unamiliki sehemu kiasi gani ndani yenu? Je, matamshi Yangu yamewagonga katika sehemu yenu ya udhaifu? Je, mnahisi kwa kweli kuwa hamna mahali pa kuficha aibu yenu? Je, mnaamini kwa kweli kuwa hamjafuzu kuwa watu Wangu? Iwapo hutambui kabisa maswali haya, basi hii inaashiria kuwa unafanya kazi gizani, kwamba uko tu pale kuongeza idadi, na kwamba katika muda ulioamuliwa na Mimi kabla ya siku hii, kwa hakika utaangamizwa na kutupwa katika shimo lisilo na mwisho kwa mara ya pili. Haya ni maneno Yangu ya onyo, na yeyote anayeyachukulia kwa wepesi atapigwa na hukumu Yangu, na, kwa wakati ulioteuliwa atapatwa na janga. Sivyo? Je, bado Ninahitaji kutoa mifano ili kueleza hili? Je, inanilazimu kuzungumza kwa uwazi zaidi ili Niweke kigezo kwa ajili yenu? Tangu wakati wa uumbaji mpaka sasa, watu wengi wamekosa kutii maneno Yangu na hivyo wametupwa nje na kutolewa katika mtiririko wa urejesho Wangu; hatimaye, miili yao inaangamia na roho zao zinatupwa kuzimu, na mpaka wa leo bado wanapitia adhabu kali. Watu wengi wameyafuata maneno Yangu, lakini wameenda kinyume na nuru na mwanga Wangu, na hivyo wametupwa kando na Mimi, wakaanguka katika miliki ya Shetani na kuwa wale wanaonipinga. (Leo hii wote wanaonipinga moja kwa moja wanatii ujuu juu wa maneno Yangu peke yake, na kuasi kiini cha maneno Yangu.) Kumekuwa na wengi, pia, ambao wameyasikiza tu maneno Niliyonena jana, ambao wameshikilia vikorokoro vya kale na hawajathamini mazao ya siku hii. Watu hawa hawajafanywa tu wafungwa na Shetani, bali wamekuwa watenda dhambi wa milele na kuwa adui Zangu, na wananipinga moja kwa moja. Watu wa aina hii ndio viumbe Nitakaohukumu wakati wa ghadhabu Yangu kali, na leo hii wao bado ni vipofu, wakiwa bado ndani ya jela zenye giza (ambayo ni kusema, watu kama hawa wameoza, maiti zisizo na hisia ambazo zinadhibitiwa na Shetani; kwa sababu macho yao yamefunikwa na Mimi, Ninasema kuwa wao ni vipofu). Ingekuwa vema kutoa mfano kwa ajili ya kurejelea kwenu, ili mpate funzo kutoka kwa mfano huu:

Kwa kumtaja Paulo, mtafikiria historia yake, na baadhi ya hadithi kumhusu zisizo sahihi na zisizo sawa na hali halisi. Yeye alifunzwa na wazazi wake kutoka umri mdogo, na akapata uhai Wangu, na kwa sababu ya majaliwa Yangu alipata kuwa na ubora wa tabia Ninaohitaji. Akiwa na umri wa miaka 19, alisoma vitabu kadhaa kuhusu maisha; hivyo Sihadhi kueleza kwa kina kuhusu vile, kwa sababu ya ubora wake wa tabia, na kwa sababu ya nuru na mwanga Wangu, hakuweza tu kuzungumza na baadhi ya utambuzi kuhusu mambo ya kiroho, bali pia aliweza kufahamu nia Yangu. Bila shaka, hili haliachi nje muungano wa mambo ya ndani na ya nje. Hata hivyo, udhaifu wake mmoja ulikuwa kwamba, kwa sababu ya talanta zake, mara nyingi angekuwa mwepesi wa kusema maneno yasiyo ya kweli na mwenye kujigamba. Kwa sababu ya hili, kwa ajili ya kutotii kwake, ambako kwa kiasi kuliwakilisha malaika mkuu, Nilipokuwa mwili mara ya kwanza, alijaribu kabisa kuniasi Mimi. Alikuwa mmojawapo wa wale wasiojua

maneno Yangu, na nafasi Yangu katika moyo wake ilikuwa tayari imeshapotea. Watu wa aina hii moja kwa moja wanaasi uungu Wangu, na wanaangamizwa na Mimi, na wanainama na kutubu dhambi zao mwishowe tu. Hivyo, baada ya Mimi kumaliza kutumia uwezo wake—ambayo ni kusema, baada ya yeye kunifanyia kazi kwa muda fulani—alirudi tena katika njia zake za zamani, na hata ingawa hakuasi maneno Yangu moja kwa moja, alipuuza mwongozo Wangu na nuru Yangu ya ndani, na hivyo yote aliyokuwa amefanya mbeleni yalikuwa bure; kwa maneno mengine, taji la utukufu alilozungumzia lilikuwa limekuwa maneno tupu, matokeo ya mawazo yake, kwa kuwa hata leo, yeye bado yuko katika hukumu yangu katika minyororo Yangu.

Kutokana na mfano huo hapo juu inaweza kuonekana kuwa yeyote anayeniasi (na sio kuuasi tu mwili Wangu lakini la muhimu zaidi, maneno Yangu na Roho Wangu—ambayo ni kusema, uungu Wangu), anapata hukumu Yangu katika mwili wake. Wakati Roho Wangu Anakuwacha, unaporomoka kwenda chini, unateremka moja kwa moja mpaka kuzimu. Na hata ingawa mwili wako wa nyama uko duniani, wewe ni kama mtu aliye na ugonjwa wa akili: Umepoteza akili yako, na ghafla unahisi ni kama wewe ni maiti, mpaka unanisihi Niutoe mwili wako bila kungoja. Wengi wenu ambao mmejawa na Roho mnao uwezo wa kuelewa hali hii kwa undani, na Mimi sihitaji kuenda katika maelezo mengi zaidi. Katika siku zilizopita, Nilipofanya kazi katika ubinadamu wa kawaida, watu wengi walikuwa tayari wamejipima dhidi ya ghadhabu Yangu na uadhama Wangu, na tayari walijua kiasi kidogo kuhusu hekima na tabia Yangu. Leo hii, Ninazungumza na kutenda moja kwa moja katika uungu, na bado kuna baadhi ya watu ambao wanaona ghadhabu na hukumu Yangu kwa macho yao wenyewe; zaidi ya hayo, kazi muhimu ya sehemu ya pili ya enzi ya hukumu ni kuwafanya watu Wangu wote wajue matendo Yangu katika mwili moja kwa moja, na kuwafanya ninyi nyote muone tabia Yangu moja kwa moja. Ihali kwa sababu Niko katika mwili, Mimi bado ni mwenye huruma kwa udhaifu wenu. Matumaini Yangu ni kuwa hamtachukua roho, nafsi na mwili wenu kama vitu vya kuchezea, na bila kujali mvikabidhi kwa Shetani. Ni vema mthamini vyote mlivyo navyo, na kutovichukulia kama mchezo, kwa maana vitu hivyo vinahusiana na majaliwa yenu. Je, kweli mnao uwezo wa kuyaelewa maneno Yangu? Je, kweli mnao uwezo wa kujali hisia Zangu za kweli?

Je, mnayo nia ya kustarehe katika baraka Zangu duniani, baraka zilizo sawa na zile za mbinguni? Je, mko tayari kuchukua kuelewa kwao kunihusu, na kufurahia kwa maneno Yangu na ufahamu wako kunihusu, kama vitu vya thamani zaidi na vya muhimu zaidi katika maisha yenu? Je, kweli mnaweza kuwa watiifu Kwangu kikamilifu, bila fikira kwa matarajio yenu wenyewe? Je, kweli mna uwezo wa kujiruhusu kuuwawa na Mimi, na kuongozwa na Mimi, kama kondoo? Je, kunao kati yenu walio na uwezo wa kutimiza vitu kama hivi? Inawezekana kuwa wote wanaokubaliwa na Mimi na kupokea ahadi Zangu ndio wanaopokea baraka Zangu? Je, mmelewa chochote kutoka katika maneno haya? Nikiwajaribu, je, mnaweza kweli kujiweka

wenyewe katika huruma Yangu, na, katikati ya majaribu haya, mtafute nia Yangu na muelewe moyo Wangu? Mimi sitamani wewe uweze kuongea maneno mengi matamu, au utoe hadithi nyingi za kufurahisha; badala yake Ninauliza kuwa uweze kuwa na ushuhuda mzuri Kwangu, na kwamba unaweza kuingia kikamilifu na kwa kina katika hali halisi. Kama Singezungumza moja kwa moja, je, ungewacha kila kitu kilicho karibu na wewe na ukubali kutumiwa na Mimi? Je, hii siyo hali halisi Ninayohitaji? Je, ni nani aliye na uwezo wa kuelewa maana iliyo katika maneno Yangu? Ilhali Ninauliza kuwa msishushwe na wasiwasi tena, kwamba mwe msitari ya mbele katika kuingia kwenu na muelewe kiini cha maneno Yangu. Hii itazuia hali ya nyinyi kutoelewa maneno Yangu, na hali ya kutokuwa na uwazi kuhusu maana Yangu, na hivyo kukiuka amri Zangu za utawala. Natumaini kuwa mtaelewa Nia Yangu kwenu katika maneno Yangu. Msifikiri juu ya matarajio yenu tena, na mtende vile ambavyo mmeamua mbele Yangu kutii mipango ya Mungu katika kila kitu. Wale wote wanaosimama miongoni mwa kaya Yangu wanapaswa kufanya mengi kiasi wanachoweza; unafaa utoe hali yako bora zaidi kwa sehemu ya mwisho ya kazi Yangu duniani. Je, unayo nia ya kuviweka vitu vya aina hii katika matendo?

Februari 23, 1992

Sura ya 5

Wakati Roho Wangu anatoa sauti, Anaonyesha hali nzima ya tabia Yangu. Je, ninyi mnalifahamu hili? Kutolifahamu hili katika hatua hii itakuwa sawa na kunipinga moja kwa moja. Je, kweli mmeona umuhimu ulioko humu? Je, mnajua kweli juhudi kiasi gani, kiasi gani cha nguvu, Ninatumia juu yenu? Je, mnaweza thubutu kuweka wazi kile mlichofanya mbele Yangu? Na mna ujasiri wa kujiita watu Wangu usoni Mwangu—hamna hisia ya aibu, sembuse mantiki yoyote! Siku moja, watu kama hawa watafukuzwa kutoka katika nyumba Yangu. Usithubutu kunidanganya, ukifikiri kwamba umesimama kwa ajili ya ushuhuda Wangu! Je, hili ni jambo ambalo binadamu ana uwezo wa kufanya? Iwapo hakungekuwa na kitu kilichobakia katika nia na malengo yako, ungekuwa umeshika njia tofauti zamani. Je, unafikiri kuwa Sijui ni kiasi gani moyo wa binadamu unaweza kustahimili? Kuanzia wakati huu na kuendelea, katika mambo yote lazima uingie katika ukweli wa kutenda; kupiga domo tu, kama ulivyokuwa ukifanya, hakutakusaidia tena. Katika siku zilizopita, wengi wenu mlifaulu kudoea chini ya paa Langu; ni kwa sababu ya ukali wa maneno Yangu ndio umeweza kusimama imara leo. Je, unafikiri kwamba maneno Yangu huzungumzwa tu kiholela bila lengo? Haiwezekani! Mimi huangalia chini juu ya mambo yote kutoka juu, na Ninatoa mamlaka juu ya mambo yote kutoka juu. Kwa njia iyo hiyo, Nimeutuma wokovu Wangu juu ya dunia. Kamwe hakuna wakati ambapo Mimi Sitazami, kutoka mahali Pangu pa siri, kila hatua ya binadamu, kila wanachosema na kutenda. Binadamu Kwangu wako wazi kabisa: Mimi Nawaona na kuwajua kila mmoja. Mahali hapo pa

siri ni makaazi Yangu, na mbingu ndiyo kitanda ambamo Mimi hujilaza. Nguvu za shetani haziwezi kunifikia, kwa maana Mimi nimejawa na uadhama, haki na hukumu. Siri isiyoelezeka imo katika maneno Yangu. Wakati Naongea, mnakuwa kama ndege waliotupwa majini, wakazidiwa na kuchanganyikiwa, au watoto ambao wamepatwa na hofu hivi karibuni, wakionekana kutojua lolote, kwa sababu roho zenu imeingia katika hali ya bumbuazi. Kwa nini Nasema kwamba mahali pa siri ni makaazi Yangu? Je, unajua maana ya ndani ya yale Ninayosema? Ni nani katika ya binadamu wote ana uwezo wa kunijua Mimi? Nani ana uwezo wa kunijua Mimi kama vile anavyomjua baba yake na mama yake? Ninapopumzika katika makaazi Yangu, Mimi huchunguza kwa karibu: Watu wote duniani wamo katika pilkapilka, “wakisafiri duniani kote” na kukimbia huku na kule, yote kwa ajili ya hatima yao, maisha yao ya baadaye. Lakini hakuna hata mmoja ana nguvu ya kutosha kwa ajili ya kujenga ufalme Wangu, hata nguvu kiasi ambayo mtu hutumia kuvuta pumzi. Mimi Niliumba wanadamu, na Nimewaokoa mara nyingi kutoka katika dhiki, lakini hawa binadamu wote ni wasio na shukrani: Hakuna hata mmoja miongoni mwao anayeweza kuhesabu matukio yote ya wokovu Wangu. Imekuwa miaka mingapi, zimekuwa karne ngapi tangu kuumbwa kwa dunia mpaka siku ya leo, na ni miujiza ngapi Niliyofanya, mara ngapi Nimeweka wazi hekima Yangu? Lakini mwanadamu, kama mwendawazimu anayeteseka na kichaa na ulegevu au, wakati mwingine kama mnyama mwitu anayeputa huku na kule katika msitu, hana nia hata kidogo ya kuyajali mambo Yangu. Mara nyingi Nimempa mwanadamu hukumu ya kifo na kumhukumu afe, lakini mpango wa usimamizi Wangu hauwezi kubadilishwa na mtu yeyote. Kwa hivyo mwanadamu bado yuko katika mikono Yangu, akiegemea vile vitu vya kale anavyokwamilia. Kwa sababu ya hatua za kazi Zangu, mimi, kwa mara nyingine tena, Nimewaokoeni, ninyi viumbe mlizaliwa katika familia kubwa zenye upotovu, uozo, uchafu, na aibu.

Kazi Niliyopanga inaendelea kusonga mbele bila kukoma hata kwa muda kidogo. Baada ya kuingia katika Enzi ya Ufalme, na baada ya kukuingiza katika ufalme Wangu kama watu Wangu, Nitakuwa na madai mengine ya kuweka dhidi yenu; hiyo ni kusema, Nitaanza kutangaza rasmi mbele yenu katiba ambayo Nitatumia kuongoza enzi hii:

Kwa sababu mnaitwa watu Wangu, mnapaswa kuwa na uwezo wa kulitukuza jina Langu, yaani, kushuhudia wakati wa majaribio. Mtu yeyote akijaribu kunirairai na kunificha ukweli, au kushiriki katika shughuli zisizo za heshima nyuma Yangu, bila ubaguzi Nitamfukuza nje, aondolewe kutoka katika nyumba Yangu akisubiri Mimi nimshughulikie. Wale ambao hawajakuwa waaminifu na wasio na upendo wa mtoto kwa mzazi Kwangu zamani, na leo hii wanainuka tena kunihukumu hadharani, wao pia watafukuzwa kutoka kwa nyumba Yangu. Wale ambao ni watu Wangu lazima wajali kuhusu mizigo Yangu kila mara na vile vile kutafuta kujua maneno Yangu. Ni watu kama hawa tu ndio Nitakaowapa nuru, na wao kwa hakika wataishi

chini ya uongozi Wangu na nuru, na kamwe hawatakutana na kuadibu. Wale ambao, kwa kutojali mizigo Yangu, wanamakinika na kupanga mustakabali yao wenyewe, yaani, wale ambao hawalengi kwa matendo yao kukidhi Moyo Wangu bali wanataka kuomba omba vya bure, viumbe hawa walio kama waombaji, Ninakataa kata kata kuwatumia, kwa sababu tangu walipozaliwa hawajui chochote kuhusu maana ya kujali mizigo Yangu. Wao ni watu wasiokuwa na akili ya kawaida; watu kama hawa wanaugua kutokana na “utapiamlo” wa ubongo, na wanahitaji kwenda nyumbani wapate “lishe.” Siwahitaji watu wa aina hii. Miongoni mwa watu Wangu, kila mtu atatakiwa kuzingatia kunijua kama wajibu wa lazima unaotakiwa kutekelezwa mpaka mwisho, kama kula, kuvaa, na kulala, mambo ambayo mtu kamwe hawezi kusahau hata kwa muda mfupi, ili kwamba mwishowe kunijua litakuwa jambo la kawaida kama vile kula, jambo ambalo wewe hufanya bila jitihada yoyote, kwa mkono uliozoea. Kuhusu maneno Ninayoyanena, kila neno lazima lichukuliwe kwa uhakika mkubwa na lichukuliwe kikamilifu; hakuwezi kuwa na hatua nusu za uzembe. Yeyote asiye kuwa makini na maneno Yangu ataonekana kama ananipinga Mimi moja kwa moja; mtu yeyote asiye yala maneno Yangu, au hatafuti kuyajua, ataonekana kama ambaye hanizingatii, na moja kwa moja atafagiliwa nje ya mlango wa nyumba Yangu. Kwa maana, kama Nilivyosema zamani, Ninachotaka sio watu wengi ila wateule wachache. Kati ya watu mia, kama mmoja tu anaweza kunijua kupitia maneno Yangu, basi bila kusita Ningewatupilia mbali wengine wote ili Nizingatie kumpa nuru na mwangaza mmoja huyu. Kutokana na hili unaweza kuona kuwa, si lazima iwe ukweli kwamba idadi kubwa pekee ndio inaweza kunidhihirisha, kuishi kulingana na Mimi. Ninachotaka ni ngano (hata ingawa viini vya mbegu huenda havijajaa) na sio magugu (hata wakati viini vya mbegu vimejaa vya kutosha kutamanika). Na kuhusu wale wasiojali kuhusu kutafuta lakini badala yake kuwa na tabia za kuzembea, wanapaswa kuondoka kwa hiari yao wenyewe; Mimi sitaki kuwaona tena, wasije wakaleta aibu kwa jina Langu. Kuhusu yale Ninayohitaji kutoka kwa watu Wangu, Nitakomea katika maagizo hayo kwa sasa, na Nitasubiri kuweka vikwazo zaidi kulingana na jinsi hali zitakavyobadilika.

Katika siku zilizopita, idadi kubwa ya watu walifikiri kuwa Mimi nilikuwa Mungu Mwenyewe mwenye hekima, kwamba mimi ndiye Nilikuwa Mungu aliyeona ndani kwa kina ya mioyo ya watu; lakini yote yalikuwa maneno ya juu juu tu. Kama mwanadamu angenijua kwa kweli, hangethubutu kufikia uamuzi bila kutafakari, ila angezidi kujaribu kunijua kupitia maneno Yangu. Wakati tu alifika katika hatua ambapo kweli angeona matendo Yangu kweli, ndipo angestahili kusema kwamba Nilikuwa mwenye Hekima, kwamba Mimi nilikuwa wa Ajabu. Ufahamu wenu kunihusu ni mdogo mno. Katika enzi zote, ni watu wangapi wamenihudumia kwa miaka mingapi, na baada ya kuona matendo Yangu, wakaja kujua kwa hakika kitu kunihusu; na basi daima wakawa na moyo wa unyenyekevu Kwangu, na kutothubutu kuwa na

nia hata kidogo ya upinzani Kwangu, kwa sababu ya jinsi ilivyo vigumu kutafuta nyayo Zangu. Kama uongozi Wangu ungekosekana miongoni mwa watu hawa, hawangethubutu kutenda bila kwa pupa, na hivyo, baada ya kuishi kwa uzoefu wa miaka mingi, hatimaye walijumlisha sehemu ya ufahamu kunihusu, wakisema kwamba Mimi ni mwenye Hekima, wa Ajabu na Mshauri, kwamba maneno Yangu ni kama upanga wenye makali pande mbili, kwamba matendo Yangu ni makuu, ya kustaajabisha, na kupendeza, kwamba Mimi Nimevikwa uadhama, kwamba hekima Yangu inafika juu kuliko anga, na ufahamu mwingine. Lakini leo mnajua tu kwa misingi ambayo waliweka, kwa hivyo idadi kubwa kati yenu, kama kasuku, mnayarudia tu maneno waliyosema. Ni kwa sababu tu Mimi huzingatia jinsi njia mnayonijua ni wa juu juu na jinsi “elimu” yako ilivyo duni ndio maana Nimewasamehe kuadibu kwingi. Lakini hata hivyo, idadi kubwa kati yenu bado hawajijui wenyewe, au mnafikiri tayari mshayafikia mapenzi Yangu katika matendo yenu, na kwa sababu hii mmeepuka hukumu. Au mnafikiri kwamba, baada ya kupata mwili, Nimekosa kujua kabisa mwelekeo wa matendo ya mwanadamu, na kwa sababu hii pia mmeepuka kuadibu. Ama mnafikiri kwamba Mungu mnayemwamini hayuko katika maeneo mapana ya ulimwengu, na kwa hivyo mmeweka kumjua Mungu kama shughuli ya kufanya wakati hamna shughuli nyingine badala ya kukuweka katika mioyo yenu kama wajibu ambao lazima utekelezwe, na kutumia imani katika Mungu kama njia ya kuchangamsha wakati ambao labda ungetumiwa kwa kuzembea. Kama Singeonea huruma ukosefu wenu wa sifa za kustahili, mantiki, na ufahamu, basi nyote mngeangamia katika kuadibu Kwangu, kutokuwepo tena. Lakini hadi wakati Kazi Yangu hapa duniani itakapomalizika, Mimi Nitabaki mwenye huruma kwa wanadamu. Hili ni jambo ambalo lazima nyote mlijue na mkome kuyachanganya mazuri na mabaya.

Februari 25, 1992

Sura ya 6

Kwa masuala ya ndani ya roho, unapaswa kuwa makini kwa utaratibu; kwa maneno Yangu, unapaswa kuwa msikivu kwa makini. Unapaswa kulenga hali ambayo unaona Roho Yangu na nafsi Yangu ya mwili, maneno Yangu na nafsi Yangu ya mwili, kama kitu kimoja kizima kisichogawanyika, na kufanya kuwa binadamu wote wataweza kuniridhisha mbele Yangu. Nimetembea ulimwenguni kwa miguu Yangu, Nikinyoosha macho Yangu juu ya anga yake nzima, na Nimetembea miongoni mwa wanadamu wote, Nikionja ladha tamu, ya asidi, chungu, na kali za uzoefu wa binadamu, lakini mwanadamu hakuwahi kweli kunitambua, wala hakuniona Nikitembea ng'ambo. Kwa sababu Nilikuwa kimya, na Sikutenda matendo yasiyo ya kawaida, kwa sababu ya hili hakuna yeyote aliyeniona kwa kweli. Mambo hayako sasa kama yalivyokuwa wakati mmoja: Naenda kufanya mambo ambayo, tangu mwanzo wa uumbaji, dunia haijawahi

kuyaona, Naenda kusema Maneno ambayo, kupitia enzi nyingi, wanadamu hawajawahi kuyasikia, kwa sababu Nauliza kwamba binadamu wote waje kunijua katika mwili. Hizi ndizo hatua kwa usimamizi Wangu, ambazo binadamu hawazijui hata kidogo. Hata Ninapozizungumzia wazi, mwanadamu bado amechanganyikiwa sana kwa akili yake mpaka haiwezekani kumwelezea kila kitu kuzihusu. Kutoka hapa kuna unyenyekevu dhalili wa mwanadamu, sivyo? Hii hasa ndiyo Nataka kurekebisha kwake, sivyo? Hii miaka yote, Sijafanya kazi yoyote kwa mwanadamu; hii miaka yote, hata waliowasiliana moja kwa moja na mwili Wangu hawakusikia sauti iliyotoka moja kwa moja kwa uungu Wangu. Na hivyo haiwezi kuepukika kwamba wanadamu wanakosa ujuzi wao Kwangu, lakini hiki kitu kimoja pekee hakijaathiri upendo wa binadamu Kwangu katika enzi. Sasa, hata hivyo, Nimekufanyia kazi nyingi ya kimiujiza na isiyoeleweka na pia kukwambia maneno mengi. Na bado, hata chini ya hali kama hizi, watu wengi bado wananipinga mbele Yangu. Wacha Nikupe mifano michache:

Kila siku unasali kwa Mungu asiye dhahiri, ukijaribu kufahamu nia Zangu, na kupata kuhisi maisha. Ilihali, mnapokabiliwa na maneno Yangu, mnayaangalia tofauti; Mnayachukua maneno Yangu na Roho Wangu kwa ujumla, ijapo mnamweka kando nafsi Yangu, mkiamini kwamba mtu Niliye hawezi kuyatamka kimsingi maneno yaliyo mfano wa haya, kwamba badala yake ni matokeo ya kupangwa na Roho Wangu. Utajuaje kuhusu hali kama hii? Unayaamini maneno Yangu kwa kadiri fulani, lakini kwa mwili Ninaovaa, kwa kiasi kikubwa au kidogo unayafikiria mawazo yako mwenyewe, unayoyatafakari siku kwa siku, ukisema: “Mbona Anafanya mambo kwa njia hiyo? Inaweza kuwa kwamba hii inatoka kwa Mungu? Haiwezekani! Kwa mtazamo wangu, Yeye ni sawa nami—mtu wa kawaida na wastani,” Tena, unawezaje kuelezea hali kama hii?

Kuhusu niliyoyasema hapo juu, kuna yeyote miongoni mwenu asiye nayo? Yeyote asiyeyamiliki? Ingeonekana kuwa kitu unachoshikilia kama kipande cha mali binafsi, na wakati huu wote umekuwa ukisita kukiachilia. Bado hujakuwa tayari kufuata juhudi amilifu; badala yake unanisubiri Nifanye kazi mwenyewe. Ukweli usemwe, hakuna binadamu hata mmoja ambaye, bila kunitafuta, anakuja kunijua kwa urahisi. Hakika, haya si maneno ya juujuu ambayo Nakuhubiria somo, kwa sababu Naweza kutoa mfano kutoka kwa pembe tofauti kwa kirejeo chako.

Punde tu anapotajwa Petro, kila mtu anajawa na sifa, akikumbushwa mara moja hizi hadithi zote kumhusu Petro—jinsi alikana kumjua Mungu mara tatu na zaidi ya hayo kumhudumia Shetani, na hivyo kumjaribu Mungu, lakini mwishowe alisulubiwa juu chini kwa ajili Yake, na kadhalika. Sasa Naweza umuhimu mkubwa juu ya kukusimulia jinsi Petro alikuja kunijua na pia matokeo yake ya mwisho. Huyu mwanadamu Petro alikuwa wa kimo bora sana, lakini hali yake ilikuwa

tofauti na ile ya Paulo. Wazazi wake walinitesa, walikuwa wa mapepo yaliyomilikiwa na Shetani, na kwa sababu hii mtu hawezi kusema kwamba walipitisha njia kwa Petro. Petro alikuwa na busara nyepesi, alipewa akili asili, kupendwa sana kutoka utotoni na wazazi wake; baada ya kukua, hata hivyo, akawa adui zao, kwani daima alitaka kunijua, na hii ilimfanya kuwapuuzwa wazazi wake. Hii ilikuwa kwa sababu, kwanza kabisa, aliamini kwamba mbingu na dunia na mambo yote yako mikononi mwa Mwenyezi, na kwamba mambo yote mazuri yanatoka kwa Mungu na yanakuja moja kwa moja kutoka Kwake, bila kupitia usindikaji wowote na Shetani. Na mfano usiofaa wa wazazi wake kuwa kama kikwazo, hii ilimwezesha kwa urahisi kutambua upendo na huruma Yangu, na hivyo kuchochea ndani yake hamu kubwa zaidi ya kunitafuta. Alikuwa makini sana sio tu kula na kunywa maneno Yangu, lakini hata zaidi kufahamu nia Zangu, na daima alikuwa na busara na tahadhari katika mawazo yake, kwa hivyo daima alikuwa mwerevu kwa makini ndani ya roho yake, na hivyo aliweza kuniridhisha kwa vyote alivyofanya. Kwa maisha ya kawaida, alikuwa makini kuunganisha katika maisha^[a] masomo ya wale walioshindwa katika siku za nyuma ili kujichochea mwenyewe kufanya juhudi kubwa zaidi, akihofia sana kwamba anaweza kuanguka ndani ya nyavu za ushinde. Alikuwa pia makini kupata imani na upendo wa wote ambao kupitia enzi nyingi walikuwa wamempenda Mungu. Kwa njia hii, aliharakisha maendeleo ya ukuaji wake sio tu kwa masuala hasi, lakini hasa kwa masuala chanya, hadi akawa katika uwepo Wangu mwanadamu pekee aliyenijua bora kabisa. Kwa sababu hii, si vigumu kuwazia jinsi alivyoweza kuweka yote aliyokuwa nayo mikononi Mwangu, kukosa kuwa tena bwana wake mwenyewe hata kwa kula, kuvaa, ama mahali aliishi, lakini alifanya kuniridhisha kwa mambo yote msingi ambao alifurahia fadhila Yangu. Mara nyingi Nilimweka chini ya jaribio, ambalo hakika lilimwacha nusu mfu, lakini hata katikati ya haya mamia ya majaribio, hakupoteza imani Kwangu hata mara moja ama kusikitishwa nami. Hata Niliposema nimemtupa kando, hakufa moyo wala kukata tamaa, lakini aliendelea kama mbeleni akitekeleza kanuni zake ili kunipenda kwa njia ya vitendo. Nilimwambia kwamba, ingawa alinipenda, Sikumsifu ila Ningemtupa katika mikono ya Shetani mwishowe. Katikati ya majaribio haya, ambayo hayakufikia mwili wake lakini yalikuwa majaribio ya njia ya maneno, bado alisali Kwangu: “Ee, Mungu! Miongoni mwa mbingu na dunia na mambo lukuki, kuna mwanadamu yeyote, kiumbe chochote, ama kitu chochote kisicho mikononi Mwako, Mwenyezi? Unapotaka kunionyesha huruma, moyo wangu unafurahishwa sana na huruma Yako; unapotaka kunihukumu, ingawa sifai, nahisi hata zaidi siri ya kushangaza ya matendo Yako, kwa sababu Umejawa na mamlaka na hekima. Ingawa mwili wangu unapitia mateso, roho yangu ina faraja. Ningewezaje kutosifu hekima Yako na matendo Yako? Hata kama nitafa baada ya kuja kukujua, kamwe nitakuwa tayari. Ee, Mwenyezi! Hakika si kwamba Wewe kweli hutaki kuniruhusu nikuone? Hakika si kwamba sistahili kweli kupokea hukumu Yako? Inaweza labda kuwa kwamba kuna kitu ndani yangu usichotaka kuona?” Katikati ya

majaribu ya aina hizi, hata kama Petro hakuweza kufahamu nia Zangu kwa usahihi, ni wazi kwamba aliliona kuwa suala la fahari na utukufu binafsi kutumiwa na Mimi (iwe tu kupokea hukumu Yangu ili binadamu waweze kuuona ukuu na ghadhabu Yangu), na hakuwa mwenye huzuni kwa ajili ya kuwekwa chini ya jaribio. Kwa sababu ya uaminifu wake mbele Yangu, na kwa sababu ya baraka Zangu juu yake, amekuwa mfano mwema na mfano wa kuigwa kwa mwanadamu kwa maelfu ya miaka. Je, huui si hasa mfano unaopaswa kufuata? Wakati huu, unapaswa kufikiria sana na kujaribu kutatua mbona Nimepeana ripoti ndefu ya Petro. Hii inapaswa kukutumikia kama kanuni ya maadili.

Hata kama kuna watu wachache sana wanaonijua, Sitatoa, kwa ajili ya hayo, hasira Yangu kwa binadamu, kwa sababu wanadamu wana dosari nyingi mpaka ni vigumu kwao kufikia kiwango ninachowauliza. Na hivyo Nimekuwa na huruma kwa binadamu kwa maelfu ya miaka, hadi wa leo. Lakini Natumai kwamba hamtakuwa tayari sana, kwa sababu ya huruma Yangu, kujishughulikia wenyewe; mnapaswa badala yake, kupitia Petro, kuja kunijua na kunitaka; kutokana na yale aliyofanya mnafaa kuangaziwa zaidi ya jinsi mlikuwa hapo awali na hivyo kufikia maeneo ambayo hayajafikiwa na mwanadamu. Kote ulimwenguni na maeneo yasiyo na kikomo ya anga, kati ya vyote vinavyopatikana mbinguni kama ilvyo duniani, vitu vyote lukuki duniani, na mambo lukuki mbinguni yote yanatoa juhudi zote kwa ajili ya ukamilisho wa kazi Yangu. Hakika hamtamani kubakia tu kama watazamaji walio kando, ambao huendeshwa hapa na pale na nguvu za Shetani? Shetani daima anagugumia maarifa ambayo wanadamu wameshikilia kunihusu mioyoni mwao, na daima, kwa meno na makucha wazi, akishiriki kwa maumivu ya mwisho ya mapambano yake ya kifo. Je, unataka kukamatwa na mipango yake danganyifu wakati huu? Unataka, wakati awamu ya mwisho ya kazi Yangu imekamilika, kukata maisha yako mwenyewe? Hakika bado hunisubiri Nisambaze huruma Yangu mara moja tena? Kutaka kunijua ni jambo muhimu, lakini hupaswi pia kupuuza kuwa makini kwa mazoezi halisi. Nafichua ufahamu kwako moja kwa moja kwa maneno Yangu, kwa matumaini kwamba utaweza kuukubali mwongozo Wangu, na kukoma kuyafikiria matarajio ama miundo yako mwenyewe.

Februari 27, 1992

Tanbihi:

a. Nakala ya awali imeacha “katika maisha yake mwenyewe.”

Sura ya 7

Matawi yote ya magharibi yanapaswa kuisikiliza sauti Yangu:

Je, mmekuwa waaminifu Kwangu hapo awali? Je, mmeyatii maneno Yangu mazuri ya

ushauri? Je, mna matumaini ambayo ni halisi na yasiyo na mashaka? Utiifu wa mwanadamu, upendo wake, imani yake—hamna kipatikanacho ila kutoka Kwangu, hamna hata kimoja ila kilichotolewa na Mimi. Enyi watu Wangu, myasikiapo maneno Yangu, je, mnaielewa nia Yangu? Mnaiona roho Yangu? Hapo zamani, mlipoipitia njia ya huduma hapo awali mlikumbana na panda shuka, maendeleo mazuri na vikwazo, na zilikuwepo nyakati mlipokuwa katika hatari ya kuanguka na hata kunisaliti Mimi; lakini mlifahamu kuwa Nilikuwa katika harakati za kuwakomboa kila wakati? Kwamba kila wakati Nilikuwa napaza sauti Yangu kuwaita na kuwaokoa? Ni mara ngapi mmeanguka katika mitego ya Shetani? Ni mara ngapi mmejiingiza katika mitego ya wanadamu? Na tena, ni mara ngapi mmejikuta katika ugomvi usio na kikomo kati yenu kwa kukosa kuziachilia nafsi zenu? Ni mara ngapi miili yenu imekuwa katika nyumba Yangu ila roho zenu zikiwa kusikojulikana? Licha ya hayo, ni mara ngapi Nimewanyooshea mkono Wangu kuwainua; ni mara ngapi Nimewaonea huruma; ni mara ngapi Nimekosa uvumilivu wa kuziona hali zenu za kuhuzunisha za mateso? Ni mara ngapi ... je, mnamfahamu?

Lakini leo kwa ulinzi Wangu, hatimaye mmezishinda shida zote na Nafurahia pamoja nanyi; hili ndilo dhihirisho la busara Yangu. Hata hivyo, likumbuke hili vyema! Ni nani kati yenu amewahi kuanguka na akaendelea kuwa thabiti? Ni nani kati yenu amewahi kuwa thabiti bila kuwa na nyakati za unyonge? Miongoni mwa wanadamu, ni nani amewahi kupokea baraka ambazo hazikutoka Kwangu? Ni nani amepitia misukosuko isiyotoka Kwangu? Inawezekana kuwa wale wote wanaonipenda hupokea baraka peke yake? Inawezekana kwamba misukosuko ilimpata Ayubu kwa sababu alikosa kunipenda ila alinikana Mimi? Inawezekana kwamba Paulo aliweza kunihudumia kwa utiifu mbele Yangu kwa sababu aliweza kunipenda kwa dhati? Ijapokuwa mnaweza kushikilia kwa uthabiti ushuhuda Wangu, lakini je, kuna mtu kati yenu aliye na ushuhuda safi kama dhahabu ambayo haijatiwa najisi? Je, mwanadamu anaweza kuwa na uaminifu halisi? Kwamba ushuhuda wenu huniletea furaha hakukinzani na “uaminifu” wenu kwa sababu Sijawahi kumtarajia mtu yeyote kutoa zaidi. Kwa kufuata dhamira asilia ya mpango Wangu, nyinyi nyote mngekuwa “bidhaa zenye kasoro”—zisizokidhi kiwango. Je, huu sio ni mfano wa kile Nilichowaambia kuhusu “kuwaonea huruma”? Je, mnachoona ni wokovu Wangu?

Nyinyi nyote mnafaa kuvuta kumbukumbu zenu: Tangu mrejee katika nyumba Yangu, kuna yeyote kati yenu, bila kutafakari faida na hasara, amenifahamu sawa na Petro alivyonifahamu? Mmekariri Biblia kikamilifu, lakini je, mlijifunza chochote kuhusu kiini chake? Japo hivyo, bado mmeshikilia “mtaji” wenu, mkikataa kuziachilia nafsi zenu. Ninapotoa tamko, Nikiwazungumzia ana kwa ana, Ni nani kati yenu amewahi kuweka chini “nyaraka” zilizofunikwa kupokea maneno ya uzima ambayo Nimeyaweka wazi? Hamyajali maneno Yangu na wala hamyathamini. Badala yake, mnatumia maneno Yangu kama bombomu dhidi ya maadui wenu ili kudumisha nafasi

zenu; hamjaribu hata kidogo kuyakubali maoni Yangu ili mnifahamu. Kila mmoja wenu anamwangazia sana mtu mwingine, nyinyi nyote ni “wasio bahili,” nyote “mnawajali wengine” katika kila hali; je, haya siyo hasa mliyokuwa mnafanya jana? Na leo je? “Utiifu” wenu umepanda juu kwa alama kidogo, na nyinyi wote mmekuwa wazoefu kiasi na mmekomaa kidogo; kwa sababu ya haya, “heshima” yenu Kwangu imeongezeka kwa kiasi fulani, na hamna hata mmoja “anatenda bila kujali.” Kwa nini mnaishi katika hali ya ubaridi wa kudumu? Ni kwa nini sifa nzuri hazipatikani kabisa ndani yenu? Enyi watu Wangu! Ya zamani yalipita kitambo; msiendelee kuyashikilia zaidi. Zamani mlishikilia msimamo wenu, leo mnapaswa kunipa utiifu wenu wa dhiti, na hata zaidi mnafaa kuwa na ushuhuda mzuri Kwangu siku za usoni, na mtarithi baraka Zangu hapo baadaye. Hili ndilo mnapaswa kufahamu.

Ingawa Siko nanyi, Roho Wangu hakika ataleta neema juu yenu. Kwa kutegemea hili, Natumaini mtaenzi baraka Yangu na mtaweza kujitambua. Msichukulie hili kuwa mtaji wenu; badala yake, mnatakiwa kujaza kinachokosekana ndani yenu kutoka katika maneno Yangu, na kutoka humu mpate mambo mazuri mnayovihitaji. Huu ndio ujumbe Ninaowaachia.

Februari 28, 1992

Sura ya 8

Ufunuo Wangu unapofika upeo wake, na hukumu Yangu inapomalizika, utakuwa wakati ambapo watu Wangu wote wanafichuliwa na kufanywa wakamilifu. Ninasafiri kila pembe ya ulimwengu dunia katika hali ya kutafuta wale wanaolingana na nia Yangu na wanastahili kwa matumizi Yangu. Nani anaweza kusimama na kushirikiana na Mimi? Upendo wa mwanadamu Kwangu ni mdogo mno na imani yake Kwangu ni ndogo ajabu. Kama sehemu kubwa ya maneno Yangu haingeelekezwa kwa udhaifu wa mwanadamu, angejigamba na kutia mambo chumvi, na angehubiri na kubuni nadharia zenye kuvutia, kana kwamba ni mwenye maarifa yote na anayejua yote kuhusu mambo ya ulimwengu. Kati ya wale waliokuwa “waaminifu” Kwangu hapo awali, na wale “wanaosimama imara” leo Yangu, ni nani anayethubutu kuongea kwa kujigamba? Nani asiye furahia matarajio yake mwenyewe kisiri? Wakati Sikufichua waziwazi, mwanadamu hakuwa na mahali pa kujificha na aliteswa na aibu. Ingekuwa mbaya zaidi kiasi gani wakati Mimi ninapozungumza kupitia mbinu nyingine? Wanadamu wangekuwa na hisia hata kubwa zaidi za kuwa wadeni, wangeamini kwamba hakuna kitu ambacho kingeweza kuwatibu, na wote wangefungwa vizuri na kutokuwa na hisia kwao. Mwanadamu anapopoteza matumaini, saluti ya ufalme husikika rasmi, ambayo ni “wakati ambapo Roho aliyeongezwa nguvu mara saba Huanza kufanya kazi,” kama ilivyosemwa na mwanadamu, kwa maneno mengine, wakati maisha ya ufalme huanza kwa urasmi duniani, yaani, wakati uungu Wangu huja kufanya kazi moja kwa

moja (bila kufikiriwa na ubongo). Watu wote wanakuwa na shughuli nyingi kama nyuki; inaonekana ni kana kwamba wamefufuliwa, kana kwamba wameamshwa kutoka ndotoni, na punde wanapoamka, wanapigwa na butwaa kwa kujikuta katika hali kama hizo. Katika siku za awali, Nilisema mengi kuhusu ujenzi wa kanisa, Nilifichua siri nyingi, na wakati ujenzi wa kanisa ulifika kilele chake, ulifika kikomo cha ghafla. Hata hivyo, ujenzi wa ufalme ni tofauti. Wakati vita katika ulimwengu wa kiroho vinapofika hatua yake ya mwisho tu ndipo Nianza upya duniani. Yaani, ni wakati tu mwanadamu anapokaribia kurudi nyuma ndipo Ninaanza rasmi na kuinua kazi Yangu mpya. Tofauti kati ya ujenzi wa ufalme na ujenzi wa kanisa ni kwamba, katika ujenzi wa kanisa, Nilifanya kazi katika ubinadamu ulioongozwa na uungu. Nilishughulika moja kwa moja na asili ya zamani ya mwanadamu, Nilifichua nafsi mbaya ya mwanadamu moja kwa moja, na kuweka wazi kiini cha mwanadamu. Kwa sababu hii, mwanadamu alikuja kujijua mwenyewe kwa msingi huu, na hivyo waliridhishwa moyoni mwao na katika neno. Katika ujenzi wa ufalme, Natenda moja kwa moja katika hali ya uungu Wangu, na kuruhusu watu wote kujua kile Nilicho nacho na Nilicho kwa msingi wa maarifa ya maneno Yangu, hatimaye kuwaruhusu kutimiza ufahamu kunihusu Mimi kama mwili halisi. Hivyo hukamilisha ufuatiliaji wote wa binadamu wa Mungu asiye dhahiri, na hivyo basi huacha kushikilia nafasi ndani ya nyoyo zao ya Mungu aliye mbinguni; yaani, Ninamruhusu mwanadamu ajue matendo Ninayotenda Nikiwa mwenye mwili, na hivyo nitahitimisha wakati Wangu duniani.

Ujenzi wa ufalme unalenga ulimwengu wa kiroho moja kwa moja. Kwa maneno mengine, vita vya ulimwengu wa kiroho vimewekwa wazi moja kwa moja miongoni mwa watu Wangu wote, na kutoka kwa hii inaweza kuonekana kwamba watu wote daima wamo vitani, sio tu katika kanisa, lakini hata zaidi katika Enzi ya Ufalme, na kwamba hata ingawa mwanadamu yuko katika mwili, ulimwengu wa kiroho unafichuliwa moja kwa moja, na mwanadamu anajihusisha na maisha ya ulimwengu wa kiroho. Hivyo, mnapoanza kuwa waaminifu, lazima mjiandae vizuri kwa ajili ya sehemu inayofuata ya kazi Yangu. Mnapaswa kutoa moyo wenu wote, na ni kwa kufanya hivi tu ndio mnaweza kukidhi moyo Wangu. Sijali kuhusu chochote ambacho mwanadamu alifanya hapo awali katika kanisa; leo, ni katika ufalme. Katika mpango Wangu, Shetani amewahi kushindana na kila hatua, na, kama foili^[a] ya hekima Yangu, amejaribu siku zote kutafuta njia na namna za kuvuruga mpango Wangu wa awali. Lakini Ningeweza kushindwa na njama zake danganyifu? Vyote mbinguni na duniani vinanitumikia—njama danganyifu za Shetani zingeweza kuwa tofauti? Huku ndiko hasa kukutana kwa hekima Yangu, ndiyo hasa yaliyo ya ajabu kuhusu matendo Yangu, na ni kanuni ya utendaji ya mpango Wangu mzima wa usimamizi. Katika enzi ya ujenzi wa ufalme, bado Mimi siepuki njama danganyifu za Shetani, ila Naendelea kufanya kazi ambayo lazima Nifanye. Kati ya ulimwengu na vitu vyote, Nimechagua matendo ya Shetani kama foili Yangu. Je, hii si hekima Yangu? Je, si haya ndiyo

hasa yaliyo ya ajabu kuhusu kazi Yangu? Wakati wa kuingia katika Enzi ya Ufalme, mabadiliko makubwa mno hutokea katika vitu vyote mbinguni na duniani, na wao husherehekea na kufurahia. Je, nyinyi mna tofauti yoyote? Ni nani asiyejisikia mtamu kama asali katika moyo wake? Ni nani asiye bubujikwa na furaha katika moyo wake? Ni nani asiyecheza kwa furaha? Ni nani asiyesema maneno ya sifa?

Katika yote Niliyonena na kusema kuhusu hapo juu, je, mnafahamu malengo na asili ya matamko Yangu, au la? Kama Singeuliza swali hili, watu wengi wangeamini kuwa Ninabubujikwa na maneno tu, na hawangeweza kutambua chanzo cha maneno Yangu. Mkiyatafakari kwa makini, mtajua umuhimu wa maneno Yangu. Ungefanya vyema kuyasoma kwa karibu: Ni yapi yasiyo ya faida kwako? Ni yapi yasiyo kwa ajili ya ukuaji wa maisha yako? Ni yapi yasiyozungumzia hali halisi ya ulimwengu wa kiroho? Watu wengi sana wanaamini kwamba hakuna maana katika maneno Yangu, ya kuwa hayana maelezo na tafsiri yoyote. Je, maneno Yangu kweli ni ya dhahania na yasiyoeleweka sana? Je, mnatii maneno Yangu kwa kweli? Je, mnayakubali maneno Yangu kwa kweli? Je, hamyachukulii kama kidude cha watoto kuchezea? Je, huyatumii kama mavazi ya kuficha sura yako mbaya? Katika dunia hii kubwa, ni nani amechunguzwa na Mimi binafsi? Ni nani ameyasikia maneno ya Roho Wangu mwenyewe? Watu wengi sana hututusa na kutafuta gizani; wengi sana huomba wakiwa kwenye shida; wengi sana, wakiwa na njaa na baridi, wengi sana wamefungwa na Shetani, ilhali wengi sana hawajui pa kugeukia, wengi sana hunisaliti wakiwa katika furaha, wengi sana hawana shukrani, na wengi sana ni waaminifu kwa njama danganyifu za Shetani. Nani kati yenu ni Ayubu? Nani ni Petro? Kwa nini Nimetaja mara kwa mara jina la Ayubu? Na mbona Nimentaja Petro mara nyingi? Je, mmewahi kufahamu matumaini Yangu kwenu? Mnapaswa kuchukua muda zaidi kuwaza mambo ya aina hii.

Petro alikuwa mwaminifu Kwangu kwa miaka mingi, lakini hakunung'unika wala kuwa na moyo wa kulalamika kamwe, na hata Ayubu hakuwa sawa na yeye. Katika enzi zote, watakatifu wote, pia, hawajamfikia hata kidogo. Yeye hakufuatilia kunijua Mimi tu, lakini pia alipata kunijua wakati ambapo Shetani alikuwa anatekeleza njama zake danganyifu. Hii ilisababisha miaka mingi ya huduma iliyopendeza nafsi Yangu, na kwa sababu hii Shetani hakumnyonya kamwe. Petro alitumia imani ya Ayubu, ilhali yeye pia alifahamu wazi upungufu wake. Ingawa Ayubu alikuwa na imani kubwa, alikosa ufahamu wa masuala katika ulimwengu wa kiroho, na hivyo alisema maneno mengi ambayo hayakulingana na hali halisi; hii inaonyesha kwamba ufahamu wake bado haukuwa wa kina, na haukuwa na uwezo wa kufanywa kuwa kamilifu. Na hivyo, Petro siku zote alitazamia kufahamu roho, na daima alilenga kuchunguza mienendo ya ulimwengu wa kiroho. Kwa sababu hii, hakuwa tu na uwezo wa kutambua matakwa Yangu kiasi, lakini pia alielewa kidogo juu ya njama danganyifu za Shetani, na hivyo ufahamu wake kuhusu

Mimi ulikuwa mkubwa zaidi kuliko mwingine wowote katika enzi zote.

Kutokana na matukio ya Petro si vigumu kuona kwamba mtu akitaka kunijua, lazima awe makini kwa kuzingatia kwa uangalifu katika roho. Sikuombi kwamba utoe kiasi kikubwa Kwangu kwa nje; hili ni la umuhimu wa ziada. Iwapo hunijui, basi imani, upendo na uaminifu wote unaozungumzia ni ndoto tu, ni upuuzi, na wewe hakika utakuwa mtu ambaye ana majivuno makubwa mbele Zangu lakini hajijui mwenyewe, na hivyo wewe utanaswa tena na Shetani na hutaweza kujinasua; utakuwa mwana wa kuteseka milele, na utakuwa mlengwa wa maangamizi. Lakini kama wewe huna hisia na hujali kuhusu maneno Yangu, basi bila shaka unanipinga Mimi. Huu ni ukweli, na ingekuwa vyema utazame kupitia lango la ulimwengu wa kiroho uone roho nyingi na tofautitofauti zilizoadibiwa na Mimi. Ni wapi kati yao hawakukaa tu na hawakujali, na hawakuyakubali maneno Yangu? Ni wapi kati yao hawakuwa na shaka kwa maneno Yangu? Ni yupi kati yao hakujaribu kutafuta makosa katika maneno Yangu? Ni wapi kati yao hawakuyatumia maneno Yangu kama silaha ya kujikinga itakayotumiwa kujilinda? Wao hawakutafuta kunijua kwa njia ya maneno Yangu, lakini waliyatumiya kama vitu vya kuchezea tu. Katika hili, je, si wao walinipinga moja kwa moja? Nani ni maneno Yangu? Nani ni Roho Wangu? Mara nyingi Mimi nimeyanena maneno haya kwenu, lakini maono yenu yamewahi kuwa ya kiwango cha juu na yenye uwazi? Matukio yenu yamewahi kuwa ya kweli? Nawakumbusha mara nyingine: Iwapo hamyajui maneno Yangu, hamyakubali, na hamyaweki katika matendo, basi bila shaka mtaadibiwa na Mimi! Nyinyi kwa hakika mtakuwa waathirika wa Shetani!

Februari 29, 1992

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Sura ya 9

Kwa sababu kwamba wewe ni mmoja wa watu nyumbani Mwangu, na kwa sababu wewe ni mwaminifu katika Ufalme wangu, kila unachofanya lazima kifikie viwango Ninavyohitaji Mimi. Sisemi kwamba uwe tu kama wingu linalofuata upepo, bali uwe kama theluji inayong'aa, na uwe na hali kama yake na hata zaidi uwe na thamani yake. Kwa sababu Nilitoka katika nchi takatifu, si kama yungiyungi, ambalo lina jina tu na halina dutu kwa sababu lilikuja kutoka katika matope na si kutoka nchi takatifu. Wakati ambapo mbingu mpya inashuka duniani na nchi mpya kuenea juu ya anga ndio pia wakati hasa ambao Ninafanya kazi kirasmi miongoni mwa binadamu. Ni nani kati ya wanadamu anayenijua Mimi? Ni nani aliyeona wakati wa kuwasili Kwangu? Ni nani ameona kwamba Mimi sina jina tu, bali zaidi ya jina Nina dutu? Mimi huyasongeza mawingu

meupe kwa mkono wangu na kwa karibu Naichunguza anga; katika anga, hakuna kitu kisichopangwa kwa mkono wangu, na chini ya anga, hakuna mwanadamu asiyechangia juhudi yake ndogo kwa ukamilishaji wa shughuli Yangu kuu. Mimi Simwekei mwanadamu madai mazito duniani, kwa maana Mimi daima Nimekuwa Mungu wa vitendo, na kwa sababu Mimi ni Mwenyezi Aliyeumba mwanadamu na Anayejua mwanadamu vizuri. Watu wote wako machoni pa Mwenyezi. Hata wale walio katika pembe zote mwisho wa dunia watawezaje kuepuka uchunguzi wa Roho Yangu? Ingawa mwanadamu “anajua” Roho Wangu, yeye pia huikosea Roho Wangu. Maneno Yangu yanaweka wazi uso mbaya wa wanadamu wote, na kuweka wazi mawazo ya ndani kabisa ya watu wote, na kusababisha wote duniani kufanywa wazi na mwanga Wangu na kuanguka chini ndani ya uchunguzi Wangu. Ijapokuwa mwanadamu anaanguka chini, moyo wake hauthubutu kwenda mbali Nami. Miongoni mwa viumbe, ni nani asiyekuja kunipenda kwa sababu ya matendo Yangu? Ni nani asiyekuwa na hamu kwa ajili ya kuyasikia maneno Yangu? Ni nani asiyezaliwa ndani mwake na hisia za ibada kwa sababu ya upendo Wangu? Ni kwa sababu tu ya ufisadi wa Shetani ndio maana mwanadamu anashindwa kuufikia ulimwengu kama Ninavyomhitaji kufika. Hata viwango vya chini kabisa ambavyo Mimi Namhitaji kufika huzalisha mashaka ndani yake, bila kutaja chochote cha leo, enzi ambayo Shetani anaendesha ghasia na ni mdhalimu mkuu, au wakati ambapo mwanadamu amekanyagwa sana na Shetani mpaka mwili wake mzima umejaa uchafu. Ni lini ambapo kutojali kwa mwanadamu kuhusu moyo Wangu kwa sababu ya upotovu wake hakujanisababishia Mimi huzuni? Je, inawezekana kwamba Mimi namwonea Shetani huruma? Je, inawezekana kwamba Mimi Nimekosea katika upendo wangu? Wakati mwanadamu ananikaidi, Moyo wangu unaomboleza kwa siri; wakati mwanadamu ananipinga, Ninamwadibu; wakati Ninamwoko mwanadamu na kumfufua kutoka wafu, Mimi Huwalisha kwa uangalifu wanaponyenyekea mbele zangu, Moyo Wangu unatulia tuli na mara moja Ninahisi mabadiliko makubwa katika mbinguni na duniani na vitu vyote. Wanadamu wanaponisifu Mimi, itawezekanaje Nisiwe na furaha? Wakati mwanadamu ananishuhudia na kupatwa na Mimi, itawezekanaje Nisitukuzwe? Inawezekana kwamba kila anachofanya mwanadamu hakiongozwi na kutolewa na Mimi? Wakati ambapo Sitoi mwelekeo, wanadamu wanazembea na kuwa wanyamavu, na, nyuma Yangu, wao wanashiriki katika zile shughuli chafu “zenye kusifika.” Je, unafikiri kwamba mwili Ninaouvaa, haufahamu chochote kuhusu matendo yako, tabia zako, na maneno yako? Nimestahimili mvua na upepo kwa miaka mingi, na vile vile Nimepitia machungu ya ulimwengu wa binadamu, lakini ukita fakari kwa karibu, hakuna kiasi cha mateso kinachoweza kumfanya mwanadamu aliye katika nyama za mwili kupoteza matumaini ndani Yangu, kama vile hakuna utamu wowote unaoweza kumfanya mwanadamu wa mwili awe bila hisia, mwenye kuvunjika moyo au mwenye kunipuuza Mimi. Je, upendo wa mwanadamu Kwangu una mipaka kwa hali ya kutokuwa na maumivu au kutokuwa na utamu?

Leo hii, Mimi niko katika nyama na nimeanza kirasmi kutekeleza kazi ambayo lazima Niifanye, na hata ingawa mwanadamu anaogopa sauti ya Roho Wangu, yeye huasi kiini cha Roho Yangu. Sihitaji kufafanua jinsi ni vigumu kwa mwanadamu kunijua Mimi Niliye katika mwili kupitia kwa maneno Yangu. Kama Nilivyosema awali, Mimi Simlazimishi mwanadamu katika matarajio Yangu, na si lazima muwe na ufahamu wote kunihusu Mimi (kwa maana mwanadamu amepungukiwa; hii ni hali asili, na ujuzi wa kujipatia hauwezi kubadili hali hii). Mnahitaji kujua tu mambo yote yanayofanyika na kusemwa na Mimi katika hali ya mwili. Na kwa maana mahitaji Yangu si ya kulazimisha, ni matumaini Yangu kwamba mnaweza kuja kujua, na kwamba mnaweza kufaulu. Lazima mjitoe katika uovu wenu kwenye ulimwengu huu mchafu, lazima mjitahidi kufanya maendeleo katika hii “jamii ya wafalme wakuu” iliyo nyuma kimaendeleo, na msijiruhusu wenyewe kuzembea. Hupaswi kujihurumia hata kidogo: Unastahili kutenga muda mwingi na kuweka juhudi ili ujue lile Nitamkalo kwa siku moja, na maarifa ya hata sentensi moja Ninayonena ina thamani ya mafunzo ya maisha marefu. Maneno Ninayonena ni yakini na dhahania, sio maneno matupu. Watu wengi wanayo matumaini ya kufaidi kutokana na maneno Yangu, lakini Siwapi sikio; watu wengi wanatamani unene Wangu, lakini Mimi Siwapi hata kidogo; watu wengi wanatamani kuuona uso Wangu, lakini kamwe Mimi nimeuficha; watu wengi husikiliza kwa makini sauti Yangu, lakini Mimi hufunga macho Yangu na kupindua Kichwa changu, kwa kuwa kutotikisika na tamaa yao; watu wengi wanahofia sauti Yangu, lakini maneno Yangu daima ni ya kuanzisha vita; watu wengi wana uoga wa kuuona uso Wangu, lakini Mimi huwatokezea kwa makusudi ili niwacharaze waanguke. Mwanadamu kwa hakika hajawahi kuuona uso Wangu na hajawahi kuisikia sauti Yangu, kwa maana yeye hanijui kwa kweli. Hata ingawa yeye anapata pigo kutoka Kwangu, hata ingawa ananiacha, hata ingawa anaadibiwa kwa mkono wangu, yeye bado hajui kama yote anayofanya ni ya kupendeza Moyo Wangu kwa kweli, na bado hana ufahamu kuhusu ni nani ambaye hufichuliwa Moyo Wangu. Tangu uumbaji wa ulimwengu mpaka sasa, hakuna mtu aliyewahi kunijua kwa kweli, au kuniona kwa kweli, na ingawa Nimekuwa mwili leo, nyinyi bado hamnijui. Je, huu sio ukweli? Je, umewahi kuona vitendo Vyangu na tabia Yangu hata kidogo katika mwili?

Mbinguni ndiko mahali Ninakojinyoosha kwenye kiti, na chini ya mbingu ndipo ambapo Mimi Hupata mapumziko. Mimi Nina mahali pa kukaa, na Ninao wakati wa kuonyesha nguvu Zangu. Kama Singekuwa duniani, kama Singejificha ndani ya mwili, na kama Singekuwa mnyenyekevu na msiri, je, si mbingu na dunia zingekuwa zimeshabadilishwa muda mrefu uliopita? Je, si nyinyi watu Wangu, mngekuwa tayari mmetumiwa na Mimi? Hata hivyo kuna hekima kwa matendo Yangu, na ingawa Ninafahamu kikamilifu kuhusu udanganyifu wa mwanadamu, Mimi Sifuati mfano wake, na badala yake Ninafanya mabadilishano nao. Hekima Yangu katika ulimwengu wa kiroho haiishi, na pia hekima Yangu katika mwili ni ya kudumu

milele. Je, huu sio wakati hasa ambao matendo Yangu yanawekwa wazi? Nimemsamehe na kufuta dhambi za mwanadamu mara nyingi, mpaka leo, katika Enzi ya Ufalme. Nitaweza kuchelewesha wakati Wangu zaidi tena? Ingawa Nimekuwa na huruma kiasi fulani kwa wanadamu mdhaifu, pindi kazi Yangu inapokamilika, Ninaweza kujiletea taabu kwa kufanya kazi ya zamani? Ningeweza kwa makusudi kumruhusu Shetani alete mashtaka? Sihitaji mwanadamu afanye kitu chochote ila kukubali ukweli wa maneno Yangu na maana halisi ya maneno Yangu. Hata ingawa maneno Yangu ni rahisi, katika kiini maneno hayo ni ngumu kufahamika, kwa maana nyinyi ni wadogo mno, na pia mmekuwa wasiosikia. Ninapozionyesha siri Zangu wazi na kufanya wazi mapenzi Yangu katika mwili, hamwoni haya yote; mnaisikiliza sauti, lakini hamwelewi maana yake. Mimi hukumbwa na huzuni kuu. Ingawa Mimi Niko katika mwili, Ninakosa uwezo wa kufanya kazi ya huduma ya mwili.

Ni nani ambaye amekuja kujua matendo Yangu katika mwili kati ya maneno na matendo Yangu? Ninapofichua siri zangu kwa maandishi, au kuzizungumza kwa sauti, watu wote hupigwa na butwaa, na wanafumba macho yao wakiwa kimya. Kwa nini Ninayosema hayaeleweki na mwanadamu? Kwa nini maneno Yangu hayaeleweki na yeye? Kwa nini yeye ni kipofu kwa matendo Yangu? Ni nani anayeweza kuniona na kamwe asiweze kusahau? Ni nani anayeweza kusikia sauti Yangu na asiiruhusu impite tu? Ni nani anayeweza kuhisi mapenzi Yangu na aufurahishe Moyo Wangu? Ninaishi na kutembea miongoni mwa wanadamu, Nimekuja kutambua wanachopitia, na ingawa Nilihisi kwamba kila kitu kilikuwa kizuri baada ya Mimi kuviumba kwa ajili ya mwanadamu, Sipati furaha kutokana na maisha miongoni mwa wanadamu, na Mimi sifurahishwi na kuwepo kwa furaha miongoni mwa wanadamu. Simchukii wala kumkataa mwanadamu, na wala Mimi Sina mvuto wa upendo kwao—kwa vile wanadamu hawanijui Mimi, wao hupata ugumu kuuona uso Wangu gizani, katikati ya kelele wanakuwa na wakati mgumu kuisikia sauti Yangu na hawawezi kutambua Ninayosema. Hivyo, kwa kijuu juu, yote mnayoyafanya ni kwa kunitii, lakini moyoni mwenu, nyinyi bado mnaniasi. Hali asili yote ya zamani ya mwanadamu, inaweza kusemwa, iko namna hii. Ni nani aliye tofauti? Ni nani asiye mmoja wa wale wanaolengwa na kuadibu Kwangu? Lakini ni nani asiyeishi chini ya uvumilivu Wangu? Kama mwanadamu angeangamizwa na ghadhabu Yangu, umuhimu wa kuumba Kwangu kwa mbingu na dunia ungekuwa nini? Wakati mmoja Niliwaonya watu wengi na kuwasih watu wengi, na kwa uwazi Nikawahukumu watu wengi—je, hili si bora zaidi kuliko kumuangamiza mwanadamu moja kwa moja? Lengo Langu sio kumweka mwanadamu kwenye mauti, bali kumfanya kujua matendo Yangu yote katika hukumu Yangu. Wakati mnapanda kutoka kuzimu, ambayo ni kusema, mnapojiweka huru kutoka kwenye hukumu Yangu, fikira zenu binafsi na mipango yote yatatoweka, na watu wote watanuia kukidhi matakwa Yangu. Na katika hili, je, Mimi Sitakuwa Nimefanikiwa katika Lengo Langu?

Sura ya 10

Enzi ya Ufalme ni, hata hivyo, tofauti na nyakati za kale. Haihusu jinsi ambavyo binadamu hutenda; badala yake, Nimeshuka duniani ili Nitekeleze kazi Yangu binafsi, jambo ambalo wanadamu hawawezi kuelewa wala kufanikisha. Kwa miaka mingi sana, tangu kuumbwa kwa ulimwengu, kazi imekuwa tu kuhusu kujenga kanisa, lakini hakuna mtu anayesikia kamwe kuhusu kujenga ufalme. Japokuwa Nazungumza kuhusu haya kwa kinywa Changu mwenyewe, yupo yeyote anayejua asili yake? Wakati mmoja Nilishuka kwenye ulimwengu wa binadamu Nikapitia na Nikaangalia kwa makini mateso yao lakini nilifanya hivyo bila ya kutimiza lengo la kupata mwili Kwangu. Punde ujenzi wa ufalme ulipoanza, Mimi nikiwa mwili nilianza rasmi kutekeleza huduma Yangu; yaani, Mfalme wa ufalme rasmi Alichukua ukuu wa mamlaka Yake makuu. Kutokana na hili ni dhahiri kwamba mshuko wa ufalme katika ulimwengu wa binadamu—mbali na kuwa tu suala la maonyesho ya moja kwa moja—ni wa ukweli halisi; hiki ni kipengele mojawapo cha maana ya “uhalisi wa kutenda.” Wanadamu hawajawahi kuona hata mojawapo ya matendo Yangu, wala hawajawahi kusikia hata mojawapo ya matamshi Yangu. Hata kama angekuwa ameona, yeye angegundua nini? Na kama angenisikia Nikiongea, yeye angeelewa nini? Kotekote katika ulimwengu, binadamu wote hukaa chini ya upendo Wangu, huruma Yangu, lakini pia binadamu wote hukaa chini ya hukumu Yangu, na vivyo hivyo chini ya majaribio Yangu. Nimekuwa mwenye huruma na upendo kwa wanadamu, hata wakati watu wote walikuwa wamepotoshwa kwa kiwango fulani; Nimegawa kuadibu kwa wanadamu, hata wakati watu wote walinyenyekea mbele ya kiti Changu cha enzi. Lakini, yupo binadamu yeyote ambaye hayuko katikati ya mateso na usafishaji Niliotuma? Ni watu wangapi wanapapasa kwenye giza kutafuta mwangaza, ni wangapi wanajitahidi kwa uchungu kupitia kwa majaribio yao? Ayubu alikuwa na imani, na hata hivyo, kwa hayo yote, hakuwa anajitafutia njia yake mwenyewe? Ingawa ninyi watu Wangu mnaweza kusimama imara katika majaribio, kunaye yeyote ambaye, bila kuongea kwa sauti, anaamini katika moyo wake? Je, si anaona ni afadhali kuongea kuhusu imani yake ilhali anaishuku moyoni mwake? Hakuna binadamu ambao wamesimama imara katika majaribio, ambao wanatoa utiifu wa kweli katika majaribio. Kama Singefunika uso Wangu ili kuepuka kuangalia dunia hii, jamii nzima ya binadamu ingeporomoka chini ya macho Yangu ya kuchoma, kwa maana Siulizi chochote kutoka kwa binadamu.

Wakati saluti kwa ufalme inapolia—ambao pia ni wakati sauti saba za radi zinanguruma—sauti hii inatetemesha mbingu na dunia, inatetemesha mbingu na kusababisha mishipa ya moyo wa kila binadamu kutetemeka. Wimbo wa taifa kwa ufalme unainuka kwa shangwe katika taifa la joka kuu jekundu, kuthibitisha kwamba Nimeliangamiza taifa la joka kuu jekundu na kisha

kuanzisha ufalme Wangu. Hata la muhimu zaidi, ufalme Wangu unaanzishwa duniani. Wakati huu, Naanza kutuma malaika Wangu kwa kila mtu wa mataifa ya dunia ili waweze kuwachunga wanangu, watu Wangu; hili pia ni kukidhi mahitaji ya hatua ya pili ya kazi Yangu. Lakini Mimi binafsi Naenda mahali ambapo joka kuu jekundu limelala likiwa limejizongomeza, Nipigane nalo. Na wakati binadamu wote wanapata kunijua Mimi kutoka ndani ya mwili, na kuweza kuyaona matendo Yangu kutoka ndani ya mwili, wakati huo makazi ya joka kuu jekundu yatageuzwa kuwa jivu na kutoweka yasipatikane tena. Kama watu wa ufalme Wangu, kwa kuwa unalichukia joka kuu jekundu katika mifupa yako, ni lazima uuridhishe moyo Wangu na matendo yako na kwa njia hii uweze kuleta aibu juu ya joka. Je, unahisi kwamba joka kuu jekundu ni lenye chuki? Je, unahisi kweli kwamba yeye ndiye adui wa Mfalme wa ufalme? Je, una imani kwa kweli kwamba unaweza kuwa na ushuhuda wa ajabu Kwangu? Je, una imani kwa kweli ya kumshinda joka kuu jekundu? Haya ndiyo Ninayotaka kutoka kwako. Yote Ninayohitaji kutoka kwako ni kwamba uweze kufika mpaka hatua hii; je, utaweza kufanya hili? Je, una imani kwamba unaweza kufikia hili? Binadamu ana uwezo wa kufanya nini? Si ni afadhali Nifanye hivyo Mwenyewe? Mbona Ninasema kwamba Mimi binafsi Nateremka mahali ambapo vita hujiunga? Ninachotaka ni imani yako, sio matendo yako. Wanadamu hawana uwezo wa kupokea maneno Yangu kwa halisi, lakini wanachungulia tu kutoka kando. Na wewe umefikia malengo haya kwa njia hii? Umekuja kunijua kwa njia hii? Kwa kusema ukweli, kati ya wanadamu walio duniani, hakuna hata mmoja aliye na uwezo wa kuniangalia Mimi moja kwa moja usoni, hakuna hata mmoja aliye na uwezo wa kupokea maana safi na nadhifu ya maneno Yangu. Na kwa hiyo Nimeweka mwendo wa kufaa usiokuwa wa kawaida wa kupanga mambo juu ya dunia, ili kufikia lengo Langu na kuanzisha mfano halisi Wangu mwenyewe katika mioyo ya watu, na kwa njia hii kutamatisha kipindi ambapo fikira huwa na mamlaka juu ya wanadamu.

Leo hii, Sishuki tu juu ya taifa la joka kuu jekundu, Mimi pia Nageuza uso Wangu kuelekea ulimwengu mzima, mpaka kila kitu cha mbingu kinatetemeka. Kunayo sehemu hata moja isiyopitia hukumu Yangu? Kunayo sehemu isiyo chini ya mateso Ninayovurumisha kuelekea chini? Kila Ninapoenda Nimesambaza “mbegu za maafa” ya kila aina. Hii ni mojawapo ya njia ambazo Nafanya kazi, na bila shaka ni kitendo cha ukombozi kwa ajili ya mwanadamu, na kile Ninachompa bado ni aina ya upendo. Nataka kufanya hata watu zaidi wapate kunijua Mimi, waweze kuniona Mimi, na kwa njia hii wapate kumcha Mungu ambaye wao hawajamwona kwa miaka mingi sana lakini ambaye, leo hii, ni halisi. Ni kwa sababu gani Niliumba dunia? Kwa sababu gani, wakati mwanadamu alipogeuka na kuwa mpotovu, Sikumwangamiza kabisa? Kwa sababu gani jamii ya wanadamu inaishi chini ya mateso? Ni kwa sababu gani Mimi Mwenyewe Niliuvaa mwili? Wakati Mimi Natekeleza kazi Yangu, binadamu haujui tu ladha ya uchungu pekee bali pia ya utamu. Kati ya watu wa dunia, ni nani asiyeishi ndani ya neema Yangu? Je,

kama Sikuwapa wanadamu baraka yakinifu, nani angeweza kufurahia utoshelevu katika ulimwengu? Hakika, kuwaruhusu kuchukua nafasi kama watu Wangu si baraka pekee Niliyowapa, sivyo? Na kama msingekuwa watu Wangu na badala yake muwe watendaji-huduma, hamngekuwa mnaishi ndani ya baraka Zangu? Hapana mmoja kati yenu anayeweza kuelewa asili ya maneno Yangu. Binadamu—mbali na kuthamini vyeo ambavyo Nimeweka juu yao, wengi wao, kwa sababu ya jina “watendaji-huduma,” wanaweka chuki katika nyoyo zao, na wengi sana, kwa sababu ya jina “watu Wangu,” huzalisha upendo Kwangu katika nyoyo zao. Hakuna anayepaswa kujaribu kunidanganya; macho Yangu huona kila kitu! Ni nani kati yenu hupokea kwa hiari, ni nani kati yenu hunipa utiifu kamilifu? Kama saluti kwa ufalme haingelia, je ungeweza kutii mpaka mwisho? Kile ambacho mwanadamu ana uwezo wa kufanya, kufikiria, anaweza kwenda umbali gani—haya yote Nimeyaamua kabla tangu kitambo.

Idadi kubwa ya watu hukubali moto Wangu katika mwanga wa uso Wangu. Idadi kubwa ya watu, wakitiwa moyo na kutumainisha Kwangu, hujiamsha wenyewe kusonga mbele katika ukimbizaji. Wakati majeshi ya Shetani hushambulia watu Wangu, Mimi Niko pale kuwakinga dhidi yao; wakati mipango ya Shetani inaleta madhara katika maisha ya watu Wangu, Nampiga akimbie kwa kujiuzulu, na asiweze kurudi tena. Duniani, kila aina ya pepo wanazungukazunguka bila mwisho wakitafuta mahali pa kupumzika, na bila kukoma wanatafuta maiti za wanadamu zinazoweza kuliwa. Watu Wangu! Lazima mbaki ndani ya utunzaji Wangu na ulinzi. Kamwe msiwahi kuishi katika hali ya upotovu! Msiwahi tenda mambo kiholela! Badala yake, salimisha uaminifu wako katika nyumba Yangu, na ni kwa uaminifu tu ndio unaweza kupinga hila ya Shetani. Katika hali yoyote usiishi kama ilivyokuwa katika siku za awali, kufanya jambo moja mbele Yangu na jingine nyuma Yangu—ukifanya hivyo umeshapita kiwango cha kukombolewa. Hakika Nimetamka zaidi ya kiasi cha kutosha maneno ya aina hii, sivyo? Ni kwa sababu asili ya mwanadamu ya zamani hairekebiki ndiyo maana Nimemkumbusha tena na tena. Usichoke! Haya yote Niyasemayo ni kwa mujibu wa kuhakikisha hatima yako! Kile Shetani anahitaji kwa hakika ni uchafu na pahali pabaya; na kadri unavyokosa kuokoleka kabisa, na kadri unavyokuwa mpotovu, ukikataa kujiwasilisha kwa hali ya kujizuia, ndivyo roho wachafu watakavyotumia nafasi yoyote ya kupenyeza. Mara unapowasili katika hii nafasi, uaminifu wako utakuwa kelele tupu, bila uhalisi wowote, na azimio lako litaliwa na pepo wachafu, kugeuzwa kuwa uasi au hila za Shetani, na kutumiwa kuzuia kazi Yangu. Kuanzia hapo, unaweza kupigwa na Mimi wakati wowote. Hakuna anayeelewa uzito wa hali hii; watu wote hupuuza tu yale wanayosikia na hawachukui tahadhari kwa vyovyote. Sikumbuki kile kilichofanywa katika siku za nyuma. Je, bado unasubiri Niwe mpole kwako Nisahau kwa mara nyingine tena? Ingawa binadamu umenipinga Mimi, Sitashikilia lolote dhidi yake, kwa maana kimo cha mwanadamu ni kidogo mno, na kwa hiyo Sihitaji makubwa kwake. Yote Ninayotaka ni kwamba yeye asijitumie

mwenyewe kwa ubadhirifu, na ajiwasilishe kwa kujizuia. Hakika si zaidi ya uwezo wako kufikia sharti hili moja? Wengi wa watu wanasubiri Nifichue mafumbo zaidi ili walishe macho yao. Ilhali, iwapo utakuja kuelewa siri zote za mbinguni, je, ni nini utakalofanya na hayo maarifa? Je, yataweza kuongeza upendo wako Kwangu? Je, yatachochea upendo wako Kwangu? Mimi Simdharau mwanadamu, wala kukata kauli kwa wepesi juu yake. Kama hizi hazingekuwa hali halisi za mwanadamu, Mimi kamwe Singewahi kamwe kuwavisha watu taji na vitambulisho hivi kwa kawaida. Fikiria kuhusu siku za nyuma: Kumekuwepo na nyakati zozote ambazo Nimewahi kuwakashifu nyinyi? Nyakati zozote ambazo Niliwadharau nyinyi? Nyakati zozote ambazo Nimekutazama bila kuzingatia hali zako halisi? Nyakati zozote ambazo Nilichosema kilishindwa kujaza moyo wako na kinywa chako na kusadiki? Nyakati zozote ambazo Nimenena bila ya kuwa na sauti ya undani ndani yenu? Ni nani kati yenu ambaye amesoma maneno Yangu bila hofu na kutetemeka, akiwa na hofu sana kwamba Nitampiga na kumwingiza kuzimu? Ni nani asiyeweza kuvumilia majaribio ndani ya maneno Yangu? Ndani ya maneno Yangu kuna mamlaka, lakini haya si ya kupitisha hukumu ya kawaida juu ya mtu; Badala yake, kwa kujali hali halisi za mwanadamu, daima Namwonyesha mwanadamu maana iliyopo katika maneno Yangu. Kwa kweli, yupo aliye na uwezo wa kutambua nguvu za kudura katika maneno Yangu? Yupo ambaye anaweza kupokea ndani ya nafsi yake dhahabu safi zaidi ambayo maneno Yangu yanaundwa nayo? Nimezungumza maneno mangapi, lakini kuna yeyote ambaye amewahi kuyathamini?

Machi 3, 1992

Wimbo wa Ufalme

Umati unanishangilia, umati unanisifu; watu wote wanalitaja jina la Mungu mmoja wa kweli, watu wote wanayainua macho yao kuviangalia vitendo Vyangu. Ufalme unashuka katika dunia ya wanadamu, nafsi Yangu ni ya fahari na yenye neema. Nani asingesherehekea kwa ajili ya hili? Ni nani asingecheza kwa ajili furaha? Ee Sayuni! Inua bendera yako ya ushindi unisherehekee! Imba wimbo wako wa ushindi ili ulieneze jina Langu takatifu! Viumbe wote hadi miisho ya dunia! Harakisheni kujitakasa ili muweze kufanywa kuwa sadaka Kwangu! Nyota juu mbinguni! Rudini kwenye maeneo yenu kwa haraka ili muonyeshe nguvu Yangu kuu katika anga! Nazisikiliza sauti za watu duniani, wanaomimina upendo na uchaji wao mwingi kwa ajili Yangu kwa nyimbo! Katika siku hii, huku viumbe wote wakirudishiwa uhai, Nashuka katika dunia ya wanadamu. Katika wakati huu, mambo yalivyo, maua yanachanua kwa wingi, ndege wote wanaimba kwa sauti moja, vitu vyote vinajawa na furaha! Kwa sauti ya saluti ya ufalme, ufalme wa Shetani unaanguka, ukiangamizwa katika mngurumo wa wimbo wa ufalme, usiinuke tena kamwe!

Nani duniani anathubutu kuinuka na kupinga? Ninaposhuka duniani Naleta moto, Naleta ghadhabu, Naleta maafa ya aina yote. Falme za dunia sasa ni ufalme Wangu! Juu angani, mawingu yanagaagaa na kujongea kama mawimbi; chini ya anga, maziwa na mito inatapakaa na kutoa muziki wa kusonga kwa furaha. Wanyama wanaopumzika wanaibuka kutoka kwenye matundu yao, na watu wote ambao wamelala wanaamshwa na Mimi. Siku ambayo watu wengi wameingojea hatimaye imefika! Wananiimbia nyimbo nzuri sana!

Katika wakati huu mzuri, katika wakati huu wa kisisimua,

sifa zinasikika kila mahali, juu mbinguni na chini duniani. Nani asingesisimka kwa ajili ya hili?

Ni moyo wa nani usingechamka? Ni nani asingelia kwa sababu ya tukio hili?

Anga si anga ya zamani, sasa ni anga ya ufalme.

Dunia si dunia ya awali, sasa ni nchi takatifu.

Baada ya mvua kubwa kupita, ulimwengu mchafu wa kale unafanywa upya kabisa.

Milima inabadilika ... maji yanabadilika ...

watu pia wanabadilika ... vitu vyote vinabadilika...

Aa, milima iliyo mitulivu! Inukeni na mnichezee!

Aa, maji yaliyotuma! Endeleni kutiririka kwa wingi!

Ninyi wanadamu mnaoota ndoto! Jiinueni na mfuate!

Nimekuja ... Mimi ni mfalme....

Wanadamu wote watauona uso Wangu kwa macho yao wenyewe, wataisikia sauti Yangu kwa masikio yao wenyewe,

watafurahia wenyewe maisha katika ufalme....

Matamu sana... mazuri sana....

Yasiyosahaulika ... yasiyoweza kusahaulika....

Katika mwako wa hasira Yangu, joka kubwa jekundu linapambana;

katika hukumu Yangu adhimu, pepo wanaonyesha sura zao za kweli;

kwa maneno Yangu makali, watu wote wanaona aibu sana, na hawana popote pa kujificha.

Wanakumbuka zamani, jinsi walivyoniidhihaki na kunikejeli.

Hakukuwahi kuwa na wakati ambapo hawakujiringa, hakukuwa kamwe na wakati ambapo hawakuniasi.

Leo, nani hali? Nani hahisi majuto?

Ulimwengu dunia wote umejawa machozi ...

umejaa sauti za kushangilia ... umejaa sauti za vicheko....

Furaha isiyoweza kufananishwa ... furaha isiyo na kifani....

Mvua nyepesi inatarakanya ... theluji nzito inaanguka....

Ndani ya watu, huzuni na furaha zinachanganyika ... baadhi wakicheka ...

baadhi wakilia ... na baadhi wakishangilia....

Kana kwamba watu wote wamesahau ... ikiwa haya ni majira ya kuchipua yaliyojaa mvua na mawingu,

majira ya joto yenye maua yanayochanua, majira ya kupukutika kwa majani yenye mavuno mengi,

au majira ya baridi yaliyo baridi kama barafu na jalidi, hakuna anayejua....

Angani mawingu yanaenda pepe, duniani bahari zinavurugwa.

Wana wanapunga mikono yao ... watu wanasogeza miguu yao wakicheza....

Malaika wanafanya kazi ... malaika wanachunga....

Watu wote duniani wanashughulika, na vitu vyote duniani vinazidishwa.

Sura ya 11

Kila binadamu anapaswa kukubali uchunguzi wa Roho Wangu, anapaswa kuchunguza kwa makini kila neno na kitendo chao, na, zaidi ya hayo, anapaswa kuangalia matendo Yangu ya ajabu. Mnahisi aje wakati wa kuwasili kwa ufalme duniani? Wakati Wanangu na watu Wangu wanarudi katika kiti Changu cha enzi, Naanza rasmi hukumu mbele ya kiti kikuu cheupe cha enzi. Ambayo ni kusema, Nianzapu binafsi kazi Yangu duniani, na wakati enzi ya hukumu

inakaribia tamati yake, Naanza kuelekeza maneno Yangu kwa ulimwengu mzima, na kutoa sauti ya Roho Wangu kwa dunia nzima. Kupitia maneno Yangu, Nitasafisha wanadamu na mambo yote miongoni mwa yote yaliyo mbinguni na duniani, ili nchi si chafu na fisadi tena, lakini ni ufalme takatifu. Nitatengeneza upya mambo yote, ili yatolewe kwa matumizi Yangu, na yasiwe na pumzi ya dunia tena, na yasichafuliwe na ladha ya ardhi tena. Duniani, mwanadamu ametafuta malengo na asili ya maneno Yangu, na amechunguza matendo Yangu, lakini bado hakuna aliyewahi kujua kwa kweli asili ya maneno Yangu, na hakuna aliyewahi kuona kwa kweli matendo Yangu ya ajabu. Ni leo tu, Nikujapo binafsi miongoni mwa wanadamu na kuongea maneno Yangu, ndipo mwanadamu anapata maarifa kidogo kunihusu, kutoa nafasi “Yangu” ndani ya mawazo yao, badala yake kutengeneza mahali pa Mungu wa vitendo ndani ya fahamu zake. Mwanadamu ana dhana na amejawa na udadisi; ni nani ambaye hangetaka kumwona Mungu? Ni nani ambaye hangetamani kukutana na Mungu? Lakini bado kitu pekee kilicho na nafasi ya uhakika ndani ya moyo wa mwanadamu ni Mungu ambaye mwanadamu anahisi kuwa dhahania na asiye dhahiri. Nani angetambua haya kama Singewaeleza wazi? Nani angeamini kwa kweli Mimi nipo? Kwa hakika bila shaka yoyote? Kuna tofauti kubwa kati ya “Mimi” aliye ndani ya mwanadamu na “Mimi” wa ukweli, na hakuna anayeweza kuwalinganisha. Nisingekuwa mwili, mwanadamu hangewahi Nijua, na hata angekuja kunijua, je, maarifa kama hayo bado hayangekuwa dhana? Kila siku Natembea miongoni mwa watu wengi, na kila siku Nafanya kazi ndani ya kila mtu. Wakati mwanadamu kweli ananiona, ataweza kunijua kwa maneno Yangu, na kuelewa njia Ninazotumia kuzungumza na pia nia Zangu.

Ufalme ufikapo rasmi duniani, ni nini, kati ya mambo yote, sio kimya? Nani, kati ya watu wote, hana hofu? Natembea kila mahali katika ulimwengu dunia wote, na kila kitu kinapangwa na Mimi binafsi. Wakati huu, nani asiyejua vitendo Vyangu ni vya ajabu? Mikono Yangu inashikilia mambo yote, lakini bado Niko juu ya mambo yote. Leo, si kupata mwili Kwangu na kuwepo Kwangu binafsi miongoni mwa wanadamu maana ya ukweli ya unyenyekevu na kujificha Kwangu? Kwa nje, watu wengi wananipongeza kama mzuri, wananisifu kama mzuri, lakini ni nani anayenijua kweli? Leo, mbona Nauliza kuwa mnijue? Lengo Langu sio kuaibisha joka kubwa jekundu? Sitaki kumlazimisha mwanadamu kunisifu, lakini kumfanya anijue kupitia hapo atakuja kunipenda, na hivyo kunisifu. Sifa kama hiyo inastahili jina lake, na si mazungumzo yasiyokuwepo; ni sifa tu kama hii inaweza kufikia kiti Changu cha enzi na kupaa angani. Kwa sababu mwanadamu amejaribiwa na kupotoshwa na Shetani, kwa sababu amechukuliwa na fikira na kuwaza, Nimekuwa mwili ili kuwashinda binafsi wanadamu wote, kufichua dhana zote za mwanadamu, na kupasua mawazo ya mwanadamu. Matokeo yake ni kuwa mwanadamu hajionyeshi mbele Yangu tena, na hanitumikii tena akitumia dhana zake

mwenyewe, na hivyo, “Mimi” katika dhana za mwanadamu ameondoka kabisa. Ufalme ufikapo, Naanza kwanza hatua hii ya kazi, na Nafanya hivyo miongoni mwa watu Wangu. Sababu nyinyi ni watu Wangu waliozaliwa kwa nchi ya joka kubwa jekundu, kwa hakika hakuna tu hata kidogo, ama kipimo cha sumu ya joka kubwa jekundu ndani yenu. Hivyo, hatua hii ya kazi Yangu hasa inawaangazia, na hiki ni kipengele kimoja cha umuhimu wa kupata mwili Kwangu Uchina. Watu wengi hawawezi kuelewa hata chembe cha maneno Ninayoyasema, na wanapoweza, uelewa wao ni wenye ukungu na ovyo. Hii ni ile hatua ya kugeuka amabayo Ninaizungumzia. Iwapo watu wote wangeweza kusoma maneno Yangu na kuelewa maana yao, basi nani miongoni mwa wanadamu angeweza okolewa, na kutupwa kuzimu? Mwanadamu anijuapo na kunitii ndio wakati Nitakapopumzika, na itakuwa wakati hasa ambapo mwanadamu ataweza kuelewa maana ya maneno Yangu. Leo, kimo chenu ni kidogo sana, karibu kiwe kiwango cha kusikitisha, na hakistahili hata kuinuliwa—sembuse ujuzi wenu kunihusu.

Ingawa Nasema malaika wameanza kutumwa mbele kuchunga wana na watu Wangu, hakuna anayeweza kuelewa maana ya maneno Yangu. Nikujapo binafsi miongoni mwa binadamu, malaika wanaanza wakati huo huo kazi ya uchungaji, na wakati huo wa uchungaji wa malaika, wana na watu wote hawapati tu majaribio na uchungaji, lakini wanaweza pia kuona, na macho yao, tukio la kila aina ya maono. Kwa sababu Nafanya kazi moja kwa moja kwa uungu, kila kitu kinaingia katika mwanzo mpya, na kwa sababu uungu huu unafanya kazi moja kwa moja, hauzuiliwi hata kidogo na ubinadamu, na unaonekana kwa binadamu kufanya kazi huru chini ya hali isiyo ya kawaida. Lakini bado, Kwangu, yote ni kawaida (mwanadamu anaamini si ya kawaida kwa sababu hajawahi kukutana na uungu moja kwa moja); hauna fikira zozote za kibinadamu, na haujachafuliwa na mawazo ya kibinadamu. Watu wataona haya wakati tu wote wataingia katika njia sawa; kwa sababu sasa ndio mwanzo, inapokuja suala la kuingia kwake, mwanadamu ana mapungufu mengi, na makosa kama haya na upofu huwezi ukaepukwa kwa urahisi. Leo, sababu Nimewaongoza hadi hapa, Nimefanya mipango ya kufaa, na Nina malengo Yangu Mwenyewe. Ningewaeleza kuyahusu leo, mngeweza kweli kuyajua? Nayajua vizuri mawazo ya akili ya mwanadamu na matakwa ya moyo wa mwanadamu: Nani hajawahi kutafuta njia ya kujitoa mwenyewe? Nani hajawahi fikiria matarajio yake mwenyewe? Lakini hata kama mwanadamu ana akili tajiri na wa mche nani aliweza kutabiri kwamba, kufuatia enzi, sasa kungekuwa kulivyo? Hili kweli ni tunda la juhudi zako binafsi? Haya ni malipo ya kazi yako ya bidii? Hii ndiyo picha nzuri iliyoonwa na akili yako? Nisingewaongoza wanadamu wote, nani angeweza kujitenga na mipango Yangu na kupata njia nyingine ya kutoka? Ni fikira akilini mwa mwanadamu na tamaa yake ambayo yamemleta hadi leo? Watu wengi wanaishi maisha yao yote bila kutimiziwa kwa matakwa yao. Kweli hili ni kwa sababu ya kosa katika fikira zao? Maisha ya watu wengi yamejawa na furaha na ridhaa isiyotarajiwa. Kweli ni kwa sababu wanatarajia

kidogo sana? Je, nani kati ya wanadamu wote hatunzwi mbele ya macho ya Mwenyezi? Nani haishi maisha kati ya majaaliwa ya Mwenyezi? Je, kuishi kwa mwanadamu kifo chake kinatokana na uchaguzi wake mwenyewe? Je, mwanadamu anadhibiti hatima yake? Wanadamu wengi wanalilia kifo, lakini kiko mbali nao; watu wengi wanataka kuwa watu wenye nguvu maishani na wanahofia kifo, lakini bila kujua kwao, siku ya kufa kwao inasongea karibu, ikiwatumbukiza ndani ya dimbwi la kifo; watu wengi wanatazama angani na kutoa pumzi kwa undani; watu wengi wanalia sana, wakiomboleza; watu wengi wanaanguka kuwapo majaribu; na watu wengi wanakuwa wafungwa wa majaribu. Ingawa Sijitokezi binafsi kumruhusu mwanadamu kunitazama vizuri, watu wengi wanaogopa kuona uso Wangu, wanaogopa sana Nitawapiga chini, kwamba Nitawaangamiza. Mwanadamu kweli ananijua Mimi ama hanijui? Hakuna anayeweza kusema kwa hakika. Sivyo? Mnaniogopa na pia kuadibu Kwangu, lakini bado mnasimama na kunipinga wazi na kunihukumu hadharani. Sivyo? Kwamba mwanadamu hajawahi kunijua ni kwa sababu hajawahi kuuona uso Wangu ama kuisikia sauti Yangu. Hivyo, hata kama Niko ndani ya moyo wa mwanadamu, je, kuna wale ambao Sionekani mwenye ukungu na asiye dhahiri katika mioyo yao? Kuna wale Ninaoonekana vizuri ndani ya mioyo yao? Sitamani wale walio watu Wangu pia kutiona vizuri, na hivyo Naanza kazi hii kubwa.

Nakuja polepole miongoni mwa wanadamu, na Naondoka taratibu. Kuna aliyewahi kuniona? Jua linaweza kuniona kwa sababu ya moto wake unaochoma? Mwezi unaweza kuniona kwa sababu ya uwazi wake unaong'aa? Kundinyota zinaweza kuniona kwa sababu ya mahali zipo angani? Nikujapo, mwanadamu hajui, na mambo yote yanabakia gizani, na Niondokapo, bado mwanadamu hafahamu. Nani anaweza kuwa na ushuhuda Kwangu? Inaweza kuwa sifa ya watu wa dunia? Inaweza kuwa mayungiyungi yanayochanua porini? Inaweza kuwa ndege wanaoruka angani? Inaweza kuwa simba wanaonguruma milimani? Hakuna anayeweza kunishuhudia kikamilifu. Hakuna anayeweza kufanya kazi Nitakayoifanya! Hata kama wangepanya kazi hii, ingekuwa na athari gani? Kila siku Naona vitendo vyote vya watu wengi, na kila siku Nachunguza mioyo na akili za watu wengi; hakuna aliyewahi kutoroka hukumu Yangu, na hakuna aliyewahi kuachana na uhalisi wa hukumu Yangu. Nasimama juu ya mawingu na kuangalia kwa umbali: Nimewaangamiza watu wengi, lakini pia watu wengi wanaishi katika huruma, na wema Wangu. Nyinyi pia hamuishi chini ya hali kama hizi?

Machi 5, 1992

Sura ya 12

Wakati umeme unatoka Mashariki—ambao pia ni wakati hasa Naanza kutamka maneno Yangu—umeme unapotoka, mbingu yote inaangazwa, na mabadiliko yanatokea kwenye nyota

zote. Wanadamu wote wanakuwa kana kwamba wamepangwa vizuri. Chini ya mng'aro wa mwale huu wa mwangaza kutoka Mashariki, wanadamu wote wanafichuliwa katika maumbo yao ya asili, macho yao yaking'aa, wakikosa uhakika wa kile wanachopsawa kufanya, na sembuse jinsi ya kuficha sifa zao mbaya. Wao pia ni kama wanyama wanaoitoroka kutoka kwa mwangaza Wangu amabao wanakimbilia usalama katika mapango ya milimani—ilhali, hakuna hata mmoja kati yao anayeweza kufutiliwa mbali kutoka katika mwanga Wangu. Wanadamu wote wako na hofu na wasiwasi, wote wanangoja, wote wanatazama; na ujio wa mwanga Wangu, wote wanasherehekea katika siku waliozaliwa, na vilevile wote wanailaani siku waliyozaliwa. Hisia zinazopingana haziwezi kuelezeka; machozi ya kujiadhibu huunda mito, na yanabebwa mbali juu ya mvo unaofagia, kwenda mara moja yasionekane tena. Kwa mara nyingine, siku Yangu inakaribia jamii ya binadamu, mara nyingine ikiamsha jamii ya binadamu, ikiwapa binadamu hatua ya kutengeneza mwanzo mpya. Moyo Wangu unapiga na, kufuatia mdundo wa mpigo wa moyo Wangu, milima inaruka kwa furaha, maji yanacheza kwa furaha, na mawimbi, kwa wakati ufaao, yanagonga juu ya mawe ya mwamba. Ni vigumu kuonyesha kile kilicho ndani ya moyo Wangu. Nataka vitu vyote visivyo safi vichomeke na kuwa majivu Nikitazama, Nataka wana wote wa kutotii wapotee kutoka mbele ya macho Yangu, wasikawie tena katika uwepo. Sijatengeneza mwanzo mpya katika makao ya joka kubwa jekundu pekee, Nimeanza pia kazi mpya katika ulimwengu. Hivi karibuni falme za dunia zitakuwa ufalme Wangu; hivi karibuni falme za dunia zitakoma kuwepo milele kwa sababu ya ufalme Wangu, kwa sababu Nimetimiza ushindi tayari, kwa sababu Nimerejea kwa ushindi. Joka kubwa jekundu limetumia njia zote za kuweza kufikiriwa ili kuvuruga mpango Wangu, likitumaini kufuta kazi Yangu duniani, lakini Naweza kukata tamaa kwa sababu ya mbinu zake za udanganyifu? Naweza kutishwa hadi kukosa kujiamini na vitisho vyake? Hakujawahi kuwa na kiumbe hata mmoja mbinguni ama duniani ambaye Simshiki katika kiganja cha mkono Wangu; ni kiwango gani zaidi ambacho huu ni ukweli kuhusu joka kuu jekundu, chombo hiki kinachotumika kama foili^[a] Kwangu? Je, pia si kitu cha kutawaliwa na mikono Yangu?

Wakati wa kupata mwili Kwangu katika dunia ya binadamu, binadamu alifika pasipo kujua katika siku hii na usaidizi wa uongozi wa mkono Wangu, pasipo kujua akaja kunifahamu. Lakini, kuhusu jinsi ya kutembea katika njia iliyo mbele, hakuna aliye na fununu, hakuna anayejua, na bado hakuna aliye na kidokezo juu ya mwelekeo ambao hiyo njia itampeleka. Mwenyezi pekee akimwangelia ndipo yeyote ataweza kutembea njia hiyo hadi mwisho; akiongozwa tu na umeme kutoka Mashariki ndipo yeyote ataweza kuvuka kizingiti kinachoelekea katika ufalme Wangu. Miongoni mwa wanadamu, hakujawahi kuwa na yeyote ambaye ameuona uso Wangu, ambaye ameona umeme katika Mashariki; sembuse yule ambaye amesikia sauti inayotoka kwa kiti Changu cha enzi? Kwa kweli, kutoka siku za zamani, hakuna

mwanadamu hata mmoja ambaye amewasiliana na nafsi Yangu moja kwa moja; leo tu, wakati Nimekuja duniani, ndipo wanadamu wana nafasi ya kuniona. Lakini hata sasa, wanadamu bado hawanifahamu, jinsi wanavyouangalia uso Wangu na kuisikia tu sauti Yangu, lakini bila kuelewa Ninachomaanisha. Wanadamu wote wako hivi. Ukiwa mmoja wa watu Wangu, je huhisi fahari ya kina unapoona uso Wangu? Na, je, huhisi aibu kwa sababu hunifahamu? Natembea kati ya wanadamu, na Naishi kati ya wanadamu, kwa kuwa Nimekuwa mwili na Nimekuja katika ulimwengu wa binadamu. Lengo Langu sio tu kuwawezesha binadamu kuutazamia mwili Wangu; cha muhimu zaidi, ni kuwawezesha binadamu kunifahamu Mimi. Zaidi, kupitia mwili Wangu, Nitamhukumu binadamu kwa dhambi zao; kupitia mwili Wangu, Nitashinda joka kuu jekundu na kuangamiza pango lake.

Ingawa wanadamu ambao wanajaza dunia ni wengi kama nyota, Nawajua wote wazi kama Ninavyotazama kiganja cha mkono Wangu mwenyewe. Na, ingawa wanadamu ambao “wananipenda” ni wengi pia kama mchanga wa bahari, ni wachache tu ndio waliochaguliwa na Mimi: wale tu wanaotafuta mwanga unaong’aa, walio kando na wale “wanaonipenda.” Sithamini mno mwanadamu, wala Sikadiri upungufu wake; ila, Namwekea mwanadamu mahitaji kulingana na sifa zake za kiasili, na hivyo kile Ninachohitaji ni aina ya mwanadamu anayenitafuta kwa dhati—hii ni kwa ajili ya kufikia lengo Langu katika kuwachagua wanadamu. Kuna wanyama wa porini wasiohesabika milimani, lakini wote ni wapole kama kondoo mbele Zangu; mafumbo yasiyoeleweka yako chini ya bahari, lakini yanajiwakilisha Kwangu wazi kama vitu vyote vilivyo katika uso wa dunia; katika mbingu juu kuna ulimwengu ambao mwanadamu hawezi kufikia kamwe, ilhali Natembea kwa uhuru katika malimwengu hayo yasiofikika. Mwanadamu hajawahi kunifahamu katika mwanga, lakini ameniona tu katika ulimwengu wa giza. Huko katika hali sawa kabisa na hiyo leo? Ilikuwa katika kilele cha ghasia ya joka kuu jekundu ndipo Nilivaa kirasmi mwili ili kufanya kazi Yangu. Ulikuwa wakati ambapo joka kuu jekundu lilifichuliwa maumbile yake ya kweli kwa mara ya kwanza ndipo Nilipokuwa na ushuhuda kwa jina Langu. Nilipotembea katika barabara za binadamu, hakuna kiumbe hata mmoja, hata mtu mmoja, aliyebumburushwa hadi kuamka, kwa hivyo Nilipokuwa mwili katika ulimwengu wa mwanadamu, hakuna aliyejua. Lakini wakati, Nikiwa katika mwili Wangu, Nilianza kufanya kazi Yangu, halafu binadamu wakaamka, walibumburushwa kutoka kwa ndoto zake na sauti Yangu ya radi, na kutoka wakati huu wakaanza maisha chini ya uongozi Wangu. Kati ya watu Wangu, Nimeanza tena kwa mara nyingine kazi mpya. Baada ya kusema kazi Yangu duniani haijaisha, hii ni toshelezi kuonyesha kuwa watu Wangu niliowazumgumzia sio wale Ninaohitaji moyoni Mwangu, lakini hata hivyo, bado Nachagua baadhi kati yao. Ni Dhahiri kutoka kwa hili kwamba Siwawezeshi watu Wangu kumjua Mungu mwenye mwili tu, bali pia kuwatakas. Kwa sababu ya ukali wa amri Zangu za utawala, watu wengi bado wako katika hatari ya kuondolewa

na Mimi. Isipokuwa ukifanya juhudi zote kujishughulikia, kuushinda mwili wako mwenyewe—isipokuwa ukifanya haya, utakuwa bila shaka kitu Ninachodharau na kukataa, cha kutupwa chini kuzimu, kama jinsi Paulo alivyopokea adabu moja kwa moja kutoka kwa mikono Yangu, ambapo hakukuwa na kutoroka kutoka hapo. Je, pengine umegundua kitu kutoka kwa maneno Yangu? Kama hapo awali, bado ni nia Yangu kulitakasa kanisa, kuendelea kuwatakaswa watu Ninaohitaji, kwani Mimi ni Mungu Mwenyewe, ambaye ni mtakatifu na safi kikamilifu. Nitafanya hekalu Langu lisiwe tu lenye rangi aina tofauti na rangi za upinde wa mvua, lakini pia liwe na usafi usiokuwa na doa, na ndani kufanane na nje yake. Katika uwepo Wangu, lazima nyote mfikirie nyuma kuhusu kile ambacho mmefanya hapo awali, na kuamua kama leo, mnaweza kuamua kunipa utoshelezo kamili katika moyo Wangu.

Mwanadamu hanifahamu Mimi tu katika mwili Wangu; zaidi ya haya, ameshindwa kuielewa nafsi yake mwenyewe inayoishi katika mwili. Kwa miaka mingi wanadamu wamekuwa wakinidanganya, wakinichukua kama mgeni kutoka nje. Mara nyingi sana, wamenifungia nje ya milango ya nyumba zao”; mara nyingi sana, wakiwa wamesimama mbele Yangu hawajanisikiliza; mara nyingi sana wamenikana miongoni mwa wanadamu wengine; mara nyingi sana wamenikana mbele za ibilisi; na mara nyingi sana, wamenishambulia kwa midomo yao ya kugombanagombana. Ilhali siweki rekodi ya unyonge wa mwanadamu, wala kwa sababu ya kutotii kwake Sijataka kulipiza kisasi. Yote ambayo Nimefanya ni kuweka dawa kwa magonjwa yake, ili kutibu magonjwa yake yasiyotibika, hivyo kumrudisha kwa afya, ili mwishowe aje kunifahamu Mimi. Yote ambayo Nimefanya si kwa ajili ya kuishi kwa binadamu, kwa ajili ya kuupa binadamu fursa ya maisha? Mara nyingi Nilikuja katika ulimwengu wa wanadamu, lakini wanadamu, kwa sababu Nilikuja Mimi Mwenyewe katika dunia, hawakujishughulisha nami; badala yake, kila mmoja alitenda kama alivyopenda, na alijitafutia suluhisho. Ila hawajui kuwa kila moja ya barabara chini ya mbingu inatoka kwa mikono Yangu! Ila hawajui kuwa kila kitu kilichoko chini ya mbingu kinakabiliwa na uratibu Wangu! Yupi kati yenu anathubutu kuhifadhi chuki katika moyo wake? Yupi kati yenu anathubutu kwa urahisi kufikia makubaliano? Nimekuwa Nikiendelea na kazi Yangu kwa kimya miongoni mwa binadamu, ni hayo tu. Kama, katika wakati wa kupata mwili Kwangu, Singekuwa mwenye huruma kwa udhaifu wa mwanadamu, basi binadamu wote, kwa sababu ya kupata Kwangu mwili, wangetishwa kabisa, na kwa sababu hiyo, ungeingia kuzimu. Ni kwa sababu tu Nilijinyenyekeza na kujificha mbali ndiyo binadamu wameepuka janga, wakapata ukombozi kutoka kwa kuadibu Kwangu, na kwa namna hii ukafika leo. Ukizingatia ilivyokuwa vigumu kufika leo, je, si ni heri uihifadhi kwa upendo mkubwa sana kesho ambayo haijafika bado?

Machi 8, 1992

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Sura ya 13

Dhamira Zangu kadhaa zimefichwa ndani ya matamshi ya sauti Yangu. Ila mwanadamu hajui na hafahamu chochote kuhusu haya, huku akiendelea kuyapokea na kuyafuata maneno Yangu kutoka nje, bila kung'amua roho Yangu na kuelewa mapenzi Yangu kutoka ndani ya maneno Yangu. Hata ingawa Nimeyaweke maneno Yangu wazi, kuna yeyote aliyelewa? Nilitoka Sayuni Nikaja miongoni mwa wanadamu. Kwa sababu Nimejivisha ubinadamu wa kawaida na ngozi ya mwanadamu, watu hilitambua umbo Langu tu kwa nje—ila hawatambui uhai uliomo ndani Yangu, wala hawatambui Mungu Roho, wanajua tu mtu wa mwili. Je, yawezekana kuwa Mungu halisi Mwenyewe hana thamani kwenu kujaribu kumfahamu? Yawezekana kuwa Mungu halisi Mwenyewe hana thamani kwenu kujaribu “kumhakiki kwa makini”? Nachukizwa na upotovu wa ukoo mzima wanadamu, lakini Nauonea imani unyonge wao. Vilevile Nashughulikia tabia ya zamani ya wanadamu. Kama mmoja wa watu Wangu katika Uchina, nyinyi si sehemu ya ukoo wa binadamu? Miongoni mwa watu Wangu wote, na miongoni mwa wanangu wote, yaani, miongoni mwa wale Niliowachagua kutoka kwa wanadamu wote, nyinyi ni wa kundi la chini zaidi. Kwa sababu hii, Nimegharamika kwa nguvu nyingi zaidi kwenu, na juhudi nyingi. Je, bado hamyathamini maisha ya baraka mnayofurahia leo? Je, bado mnafanya mioyo yenu kuwa migumu na kuasi dhidi Yangu na kuenenda katika mipangilio yenu wenyewe? Isingekuwa kwa ajili ya huruma na upendo Wangu, binadamu wote wangukuwa wameshakuwa mateka wa Shetani na kugeuka kuwa “mafunda matamu” katika kinywa chake. Leo hii, miongoni mwa binadamu wote, wale wanaotumia rasilimali kwa dhati kwa ajili Yangu na wale wanaonipenda kwa dhati ni adimu sana kiasi cha kuwahesabu kwa vidole vya mkono mmoja. Yawezekana kuwa jina “watu Wangu” limekuwa miliki yenu binafsi? Je, dhamiri yako imeingia ubaridi? Je, unafaa kweli kuwa mtu Ninayehitaji? Kwa kutafakari kuhusu zamani, halafu sasa, ni nani kati yenu ameufurahisha moyo Wangu? Ni nani kati yenu ameonyesha kutaka kujihusisha kwa kweli kwa nia Zangu? Kama Mimi Singewazindua, bado msingeamka, lakini, mngeendelea kuwa kama mlioganda, na tena, kana kwamba katika hali ya kubumbwaa.

Katikati ya mawimbi mabaya, mwanadamu huiona ghadhabu Yangu; katika dhoruba na mawingu meusi, wanadamu huogopeshwa kiasi cha kuwa na wazimu, wasijue pa kukimbilia, kana kwamba radi na mvua zitawasomba. Kisha, baada ya kupita kwa dhoruba ya theluji, hali zao zinakuwa tulivu na zenye furaha wanavyopendezwa na urembo wa mandhari ya asili. Lakini, katika wakati huo, ni nani kati yao amewahi kushuhudia mapenzi Yangu yasiyo na kikomo

Niliyo nayo kwa binadamu? Katika mioyo yao ni umbo Langu tu, ila si kiini cha Roho Wangu: Yawezekana kwamba mwanadamu hanikatai hadharani? Tufani ikishapita wanadamu wote huwa kama walitengezwa upya, kana kwamba, kufuatia usafishaji kupitia taabu, wamepata mwangaza na uhai. Je, hamkuwa na bahati njema kufika leo baada ya kupitia mapigo yote Niliyowapa? Lakini leo ikiisha na kesho kuwadia, mtaweza kuendelea kudumisha utakatifu uliofuata mvua hiyo? Mtaweza kuendelea kuwa na moyo wa ibada uliofuata usafishaji wenu? Mtaendelea kuwa na utiifu wa leo? Ibada yenu yaweza kuendelea kuwa imara au kubadilika? Kwa hakika hili si sharti lililo nje ya uwezo wa mwanadamu. Ninaishi na wanadamu siku baada ya siku Nikitenda pamoja na wanadamu, miongoni mwa wanadamu, ila hapana hata mmoja aliyegundua hili. Isipokuwa uongozi wa Roho Wangu, ni nani kati ya ukoo mzima wa wanadamu bado angekuwepo katika enzi hii? Yawezekana Ninatia chuku Ninaposema kuwa Naishi na kutenda miongoni mwa wanadamu? Zamani Nilisema kuwa “Niliwaumba binadamu, na kuwaongoza binadamu wote, na kuwaamuru binadamu wote”; hili halikuwa kweli? Inawezekana kuwa uzoefu wenu wa haya mambo ni finyu? Kauli ya “mtendaji-huduma” inafaa kukutosha kugharamia juhudi zenu maishani mkieleza kwa undani. Bila uzoefu halisi, mwanadamu hawezi kunifahamu, hangeweza kuja kunifahamu kupitia katika maneno Yangu. Hata hivyo, leo Nimekuja mwenyewe miongoni mwenu—hili halitakuwa lenye manufaa kwa kuelewa kwenu? Yawezekana kwamba kupata mwili Kwangu vilevile si ukombozi kwenu? Nisingeshuka kuja kwa mwanadamu Mimi binafsi, ukoo wote wa binadamu ungekuwa umeingiliwa na Shetani na kuwa mali yake, kwa sababu unachokiamini ni sura ya Shetani na hakihusiani na Mungu Mwenyewe kwa njia yoyote. Si huu ni ukombozi Wangu?

Shetani anapokuja mbele Yangu, sitetemeki kwa kuuogopa ukali wake, wala kumuogopa kwa sababu ya ubaya wa sura yake; Ninampuuza tu. Shetani anaponijaribu, Ninauona ujanja wake na kumfanya atoweke kwa haya na aibu. Shetani anapopigana na Mimi na kujaribu kunipokonya wateule Wangu, Ninapigana vita na yeye katika mwili Wangu; na katika mwili Wangu Nawakimu na kuwaongoza watu Wangu ili wasianguke na kupotea, na Nawaongoza katika kila hatua ya safari. Na Shetani anapong’atuka kwa kushindwa, Nitakuwa nimetukuka na watu Wangu watakuwa wamenitolea ushuhuda mzuri na mkubwa. Kwa hivyo, Nitachukua ninavyotumia kama foili^[a] katika mpango Wangu wa usimamizi na kuvitupilia mbali hatimaye katika shimo lisilo na mwisho. Huu ndio mpango Wangu; hii ndiyo Kazi Yangu. Katika maisha yenu, ipo siku itakuja ambayo utakumbana na hali kama hii: Je, utakubali bila kusita kushikwa mateka na Shetani, au utaniruhusu Nikuokoe? Haya ndiyo majaliwa yako mwenyewe, na sharti uzingatie kwa makini.

Maisha katika ufalme ni maisha ya watu na Mungu Mwenyewe. Binadamu wote wako katika ulinzi Wangu na wote wako vitani dhidi ya joka kuu jekundu. Ili kushinda hili pambano la

mwisho, ili kulimaliza kabisa hili joka kuu jekundu ni sharti watu wote wajitolee asili zao kabisa Kwangu katika ufalme Wangu. “Ufalme” unaozungumziwa hapa unaashiria maisha ambayo mtu anaishi chini ya uongozi wa uungu, ambamo Mimi ni mchungaji wa wanadamu wote, ambao wanakubali mafundisho Yangu moja kwa moja ili kwamba maisha ya binadamu wote, ingawa yupo duniani, yawe kama yu mbinguni—utambuzi wa kweli wa maisha ya mbingu ya tatu. Ingawa Niko katika mwili Wangu, Sikumbani na upungufu wa kimwili. Mara nyingi Nimekuja miongoni mwa wanadamu kusikiliza maombi, na mara nyingi Nimefurahia sifa zao ninapotentemba miongoni mwao; japo wanadamu hawajaugundua uwepo Wangu, bado Naendelea na kazi Yangu kwa njia hii. Katika makao Yangu, ambayo ni sehemu Nilipojificha, hata hivyo, katika haya makao Yangu, Nimewashinda maadui Wangu wote; katika makao Yangu, Nimepata uzoefu wa kuishi duniani; katika makao Yangu, Ninalichunguza kila neno na tendo la mwanadamu, na kuchungulia na kuongoza wanadamu wote. Binadamu wangejikusisha na dhamira Yangu, hivyo kuuridhisha moyo Wangu na kunifurahisha, kwa hakika Ningewabariki wanadamu wote. Hili silo Ninalolikusudia kwa binadamu?

Mwanadamu akiwa kwenye usingizi mzito, ni kwa mapigo ya radi Yangu tu ndipo wanaweza kuzinduka kutoka ndotoni mwao. Na wafunguapo macho yao, wengi huumizwa machoni na mwanga huu baridi, hadi kwa kiwango kwamba wanapoteza mwelekeo, na kushindwa kutambua watokako na waelekeako. Watu wengi hupigwa na mwale huu kama wa mshale na kama matokeo huanguka kwenye rundo chini ya dhoruba, na miili yao kusombwa na mafuriko, bila kuacha nyuma dalili yoyote. Katika mwangaza, manusura hatimaye huweza kuuona uso Wangu kwa uwazi zaidi, na hapo ndipo hugundua kitu kuhusu umbo Langu la nje, kwa kiasi kwamba wao hawawezi kuthubutu kuniangalia usoni ana kwa ana, wakihofu pakubwa kuwa Nitaitetea tena miili yao kuadibu Kwangu na laana. Watu wengi sana hulika kwa sauti na kwa uchungu mwingi; wengi sana hukata tamaa; wengi sana husababisha mito na damu yao; wengi huwa miili inayoelea huku na kule bila mwelekeo; watu wengi sana, wanapopata sehemu yao katika mwangaza, huhisi uchungu wa mioyo yao ghafla na kulia machozi kwa ajili ya miaka yao ya kukosa furaha. Watu wengi sana, kwa msukumo wa mwangaza huu wa kuogofya hukiri uchafu wao na kuamua kujibadilisha; wengi kwa kuwa wamepofushwa wamepoteza hamu ya kuishi na hatimaye hawawezi kamwe kuuona huu mwangaza na kwa hivyo kukwama, wakisubiri mwisho wao. Na ni watu wengi sana huanza safari ya maisha yao na, chini ya uongozi wa mwanga huu, kwa bashasha wakitumainia kesho. ... Leo hii ni nani miongoni mwa binadamu hayumo katika hali sawa na hii? Ni nani hayumo katika mwangaza Wangu? Hata kama wewe ni mwenye nguvu, au hata kama wewe ni mnyonge, unawezaje kuepuka ujio wa mwanga Wangu?

Machi 10, 1992

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Sura ya 14

Katika enzi zote, hakuna mwanadamu ameingia katika ufalme na hivyo hakuna aliyefurahia neema ya Enzi ya Ufalme, hakuna aliyeona Mfalme wa ufalme. Ingawa chini ya nuru ya Roho Wangu watu wengi wametabiri uzuri wa ufalme, wanajua tu nje ya ufalme, sio umuhimu wa ndani. Leo, ufalme ujapo kuwepo rasmi duniani, binadamu wote bado hujui kinachopaswa kukamilishwa, ulimwengu ambao binadamu hatimaye ataletwa ndani, wakati wa Enzi ya Ufalme. Kuhusu haya, Naogopa watu wote wako katika hali ya mkanganyiko. Kwa sababu siku ya utambuzi kamili wa ufalme bado haijafika kabisa, wanadamu wote wamechanganyikiwa, hawawezi kuona vizuri. Kazi Yangu ya uungu inaanza rasmi na Enzi ya Ufalme. Ni katika mwanzo rasmi wa Enzi ya Ufalme kwamba tabia Yangu inaanza kuendelea kudhihirika kwa mwanadamu. Hivyo kwa muda huu tarumbeta takatifu inaanza rasmi kutoa sauti na kutangaza kwa wote. Nichukuapo kirasmi mamlaka Yangu na kutawala kama Mfalme katika ufalme, watu Wangu wote watakamilishwa na Mimi baada ya muda. Wakati mataifa yote ya dunia yata vurugwa, hapo ndipo hasa ufalme Wangu utanzishwa na kupata umbo na pia Nitabadilika na kurejea kwa ulimwengu mzima. Wakati huo, watu wote watauona uso Wangu tukufu, watauona uso Wangu wa kweli. Tangu uumbaji wa dunia, kutokana kupotoshwa kwa watu na Shetani kufikia kiwango cha upotovu leo, imetokana na upotovu wao kiasi kwamba Nimekuwa, kwa maoni yao, Nimefichwa zaidi na zaidi kutoka kwake na Nikazidi kutoeleweka na wao. Binadamu hawajawahi kuuona uso Wangu wa kweli na hajawahi kuathiriana na Mimi moja kwa moja. Ni kwa tetesi na hadithi tu ndipo kumekuwa na “Mimi” kwa ubunifu wa mwanadamu. Kwa hivyo Nakubaliana na ubunifu wa binadamu, kwamba, ni dhana za binadamu, kukabiliana na “Mimi” kwa akili za wanadamu, kwamba Naweza kubadilisha hali ya “Mimi” ambayo wameweka kwa miaka mingi. Hii ni kanuni ya kazi Yangu. Hakuna mtu hata mmoja ameweza kuijua vizuri sana. Ingawa wanadamu wamejilaza na kuja mbele Yangu kuniabudu, Sifurahii matendo kama haya ya wanadamu kwa sababu kwa mioyo yao hawajashikilia mfano Wangu, lakini mfano ambao sio Wangu. Kwa hivyo, akili zao zinapokosa tabia Yangu, hawajui chochote kuhusu uso Wangu wa kweli. Kwa hivyo, wakati wameamini wamenipinga ama kukosea amri Zangu za kiutawala, Nitajifanya kwamba sioni. Na hivyo, kwa kumbukumbu zao, Mimi ni Mungu anayeonyesha huruma kwa wanadamu badala ya kuwaadibu, ama Mimi ni Mungu Mwenyewe asiyemaanisha Anachokisema. Haya yote ni mawazo yanayotokana na fikira za wanadamu na sio kwa mujibu na ukweli.

Siku baada ya nyingine, Nasimama kwa uchunguzi juu ya ulimwengu, na hujificha Mimi

Mwenyewe kwa unyenyekevu katika makazi Yangu nikipitia maisha ya binadamu, na kuchunguza kwa karibu matendo yote ya binadamu. Hakuna aliyewahi kujitolea Kwangu kwa kweli. Hakuna aliyewahi kufuata ukweli. Hakuna aliyewahi kuwa mwangalifu Kwangu. Hakuna aliyewahi kufanya maazimio mbele Yangu na kufanya wajibu wake. Hakuna aliyewahi kuniruhusu kuishi ndani yake. Hakuna aliyewahi kunithamini kama afanyavyo maisha yake. Hakuna aliyewahi kuona, kwa vitendo, kile ambacho uungu Wangu ni; hakuna aliyewahi kutamani kuwasiliana na Mungu wa vitendo Mwenyewe. Wakati maji yanameza wanadamu, Nawaokoa kutokana na maji yaliyotuma na kuwapa nafasi ya kuishi upya. Wanadamu wanapopoteza imani yao ya kuishi, Nawavuta juu kutoka ukingo wa kifo, na kuwapa ujasiri wa kuishi, ili kwamba wananichukua kama msingi wa kuwepo kwao. Wanadamu wanaponiasi, Nawafanya Kunijua kwa kuasi kwao. Kutokana na asili ya zamani ya binadamu na kutokana na huruma Yangu, badala ya kuwaua binadamu, Nawaruhusu kutubu na kuanza upya. Wakati wanadamu wanateseka na kiangazi, Nawatoa kifoni kama bado wamesalia na pumzi moja, kuwazuia kudanganywa na Shetani. Watu wameona mikono Yangu mara ngapi; watu wameona uso Wangu karimu mara ngapi, kuuona uso Wangu wa tabasamu; na wameona adhama Yangu mara ngapi, kuona ghadhabu Yangu. Ingawa binadamu haujawahi kunijua, Siwakamati juu ya udhaifu wao kufanya matata yasiyohitajika. Kupitia ugumu wa binadamu, Nina huruma na udhaifu wake. Ni kwa sababu ya kuasi kwa wanadamu, kutokuwa na shukrani kwao, ndiko Nawaadibu kwa viwango tofauti.

Najificha wakati wanadamu wana kazi nyingi na kujifichua wakati wao wa burudani. Binadamu unanidhania kuwa Anayejua yote na kuwa Mungu Mwenyewe anayekubali maombi yote. Wote basi wanakuja mbele Yangu kutafuta tu msaada wa Mungu, bila kuwa na tamaa ya kunijua. Wakiwa katika maumivu ya magonjwa, wanadamu wananiomba msaada. Wakiwa na shida, wananiambia matatizo yao kwa nguvu zao zote ili kumwaga mateso yao. Na bado hakuna mwanadamu hata mmoja ameweza kunipenda pia akiwa na faraja. Hakuna mtu hata mmoja amenitafuta wakati wa amani na furaha ili Nishiriki furaha yake. Wakati jamii zao ndogo zina furaha na ziko sawa, watu wameniweka kando ama kunifungia mlango, kunikataza kuingia, ili waweze kufurahia baraka za furaha za familia zao jamii. Akili ya binadamu ni nyembamba sana, nyembamba sana hata kumshikilia Mungu, appendaye, mwenye huruma, na mkunjufu kama Mimi. Nimekataliwa mara ngapi na wanadamu wakati wao wa kicheko na furaha, Nimetegemewa kama gongo mara ngapi na wanadamu wakati wanaanguka; Ni mara ngapi Nimelazimishwa kuwa daktari wa wanadamu wanaougua magonjwa. Mwanadamu ni katili jinsi gani! Hawana akili na ni wabaya kabisa. Hawana hata hisia zinazopatikana kwa binadamu. Nusura hawana ubinadamu hata kidogo. Fikiria siku za nyuma na linganisha na sasa. Kuna mabadiliko yanayofanyika ndani zenu? Kuna siku kidogo za zamani sasa? Ama zamani bado

haijabadilishwa?

Juu ya mlima na chini ya bonde Nimepitia, na kuwa na uzoefu wa panda shuka za dunia. Nimetembea na kuishi miongoni mwa wanadamu kwa miaka mingi, lakini bado inaonekana tabia ya binadamu imebadilika kidogo. Na ni kama asili ya zamani ya mwanadamu imeeneza mizizi na kuota ndani yao. Hawawezi kamwe kubadili hiyo asili ya zamani, kuiboresha tu kwa msingi wa kwanza. Wasemavyo wanadamu, kiini hakijabadilika, lakini umbo limebadilika sana. Watu wote wanaonekana wakijaribu kunidanganya na kunihadaa, ili waweze kujionyesha ili wapate kuthami na kukubaliwa na Mimi. Sipendi wala kutia maanani ujanja wa wanadamu. Badala ya kukasirika, Nachukua mtazamo wa kuangalia lakini si kuona. Napanga kuwapa binadamu kiwango fulani cha uhuru, na hivyo, kushughulikia wanadamu wote kwa pamoja. Kwa sababu wanadamu wote hawajiheshimu na ni maskini wasio na faida, wasiojithamini, watawezaje kunihitaji kuonyesha huruma na mapenzi mapya? Wanadamu wote hawajijui, na hawajui uzito wao. Wanapaswa kujipima uzito. Binadamu haunitambui, hivyo Nami pia siutilii maanani. Wanadamu hawanitambui, kwa hivyo Mimi pia Siweki juhudi kwao. Je, hii ni bora? Je, hii haiwazungumzii, watu Wangu? Nani amefanya maazimio mbele Yangu na kukosa kuyatupilia mbali baadaye? Nani amefanya maazimio ya muda mrefu mbele Yangu badala ya kutatua mara nyingi juu ya hii na hiyo? Daima, wanadamu hufanya maazimio mbele Yangu wakati wa raha na kuyafuta kabisa wakati wa shida. Baadaye, wanachukua uamuzi wao na kuuweka mbele Yangu. Je, Mimi si wa kuheshimika hadi Naweza kubali kwa kawaida taka iliyookotwa na mwanadamu kutoka pipani? Wanadamu wachache hushikilia maazimio yao, wachache ni safi, na wachache wanatoa yenye thamani kubwa zaidi kama sadaka Kwangu. Je, nyinyi wote si sawa kwa njia hii? Iwapo, kama mmoja wa watu Wangu kwenye ufalme, huwezi kufanya wajibu wenu, mtachukiwa na kukataliwa na Mimi!

Machi 12, 1992

Sura ya 15

Wanadamu wote ni viumbe wasio na ufahamu kujihusu, na hawezi kujijua mwenyewe, yeye hata hivyo anajua kila mwanadamu mwingine kama kiganja cha mkono wake, kana kwamba watu wengine wote wamepitia ukaguzi wake na kupokea kibali chake kabla waseme au kufanya chochote, na hivyo ionekane kama yeye amewapima kikamilifu wengine wote mpaka katika hali yao ya kisaikolojia. Binadamu wote wako namna hii. Mwanadamu ameingia katika Enzi ya Ufalme leo hii, lakini asili yake bado haijabadilika. Yeye bado anafanya kama Ninavyofanya akiwa mbele Yangu, lakini nyuma Yangu anaanza kufanya “shughuli” zake mwenyewe za kipekee. Hata hivyo, mara hiyo inapokamilika na anarudi mbele Yangu tena, yeye huwa kama

mwanadamu tofauti, akiwa na hali ya utulivu safihi, hali yake ni shwari, na mpigo wa moyo wake ni mtulivu. Je, si hili ndilo hasa hufanya mwanadamu kudharauliwa? Ni watu wangapi huvaa sura mbili tofauti kabisa, moja mbele Yangu na nyingine nyuma Yangu? Wangapi kati yao ni kama wanakondoo wachanga mbele Yangu lakini nyuma Yangu hugeuka na kuwa chui wabaya wenye milia wakali kinyama, na kisha kugeuka ndege wadogo wakirukaruka huku na kule kwa furaha milimani? Ni wangapi huonyesha lengo na uamuzi mbele Yangu? Ni wangapi huja mbele Zangu, kutafuta maneno Yangu kwa kiu na hamu lakini, nyuma Yangu, kukerwa nayo na kuyaacha, kana kwamba maneno Yangu ni mzigo unaosumbua? Mara nyingi, Nikiona jamii ya binadamu ikipotoshwa na adui Yangu, Mimi Nimeacha kuweka matumaini Yangu katika mwanadamu. Mara nyingi, Nikiona mwanadamu akija mbele Zangu kwa machozi akiomba msamaha, lakini kwa sababu ya kutojiheshimu kwake, utundu wake usiorekebika, Nimefunga macho Yangu kwa vitendo vyake kwa hasira, hata wakati moyo wake ni wa kweli na nia yake ni ya dhati. Mara nyingi, Naona mwanadamu akiwa na uwezo wa kuwa na imani ya kushirikiana na Mimi, ambaye, wakati ako mbele Yangu, anaonekana kuwa katika kumbatio Langu, akionja joto lake. Mara nyingi, kwa kuona upole, uchangamfu, na uzuri wa watu Wangu Niliowachagua, katika Moyo wangu Mimi daima Nimekuwa na furaha kwa sababu ya mambo haya. Binadamu hawajui jinsi ya kufurahia baraka Nilizowaamulia kabla katika mikono Yangu, kwa sababu wao hawajui ni nini hasa maana ya baraka au mateso. Kwa sababu hii, wanadamu wako mbali na kweli katika jitihada zao za kunitafuta. Kama hakungekuwa na kesho, ni yupi kati yenu mlisosimama mbele Yangu atakuwa safi kama theluji na asiye na lawama kama jiwe la thamani? Hakika upendo wako Kwangu si kitu ambacho kinaweza kubadilishwa kwa mlo wenye ladha, au suti yenye ufahari, au ofisi ya juu na mishahara mikubwa? Au inaweza kubadilishwa na upendo ambao wengine wako nao kwako? Hakika, kupitia majaribu hakutawafukuza wanadamu waache upendo wao Kwangu? Hakika, mateso na dhiki hayatasababisha mwanadamu alalamike dhidi ya kile Nimepanga? Hakuna mwanadamu aliyewahi kweli kufahamu upanga ulio katika kinywa Changu: Yeye anajua maana yake ya juu bila kufahamu undani wake. Kama wanadamu wangepata kweli kuona ukali wa upanga Wangu, wangepimbia kwa hofu hadi ndani ya mashimo kama panya. Kwa sababu ya kutokuwa kwao na hisia, wanadamu hawaelewi kitu chochote cha maana halisi ya maneno Yangu, na hivyo wao hawana kidokezo kuhusu jinsi maneno Yangu ni yenye kuogofya, au kiasi gani asili yao imefichuliwa, na ni kiasi gani cha upotovu wao umepokea hukumu, ndani ya maneno hayo. Kwa sababu hii, kulingana na mawazo yao yasiyo kamili kuhusu maneno Yangu, watu wengi wamechukua msimamo vuguvugu na usio wa kuwajibika.

Ndani ya ufalme, si tu kwamba matamko hutoka kinywani Mwangu, lakini miguu Yangu inatembea kwa heshima kila mahali katika nchi zote. Kwa njia hii, Mimi Nimepata ushindi juu

ya maeneo yote yasiyo safi na yenye uchafu sana, ili kwamba isiwe tu ni mbinguni inabadilika, lakini pia dunia iwe katika mchakato wa mabadiliko, ili ifanywe mpya muda mfupi baadaye. Ndani ya ulimwengu, kila kitu huangaza kama kipya katika mwangaza wa utukufu Wangu, kikitoa kipengele chenye kufurahisha ambacho hufurahisha akili na kuinua roho za watu, kana kwamba uko katika mbinguni iliyo zaidi ya mbingu, kama inavyodhaniwa katika fikira za binadamu, ambazo hazijanajisiwa na Shetani na zisizo na mashambulizi ya maadui wa nje. Juu ulimwenguni, nyota lukuki zinachukua maeneo yao mateule kwa amri Yangu, zikitoa mwanga wao kupitia sehemu za nyota katika wakati wa giza. Hakuna kiumbe hata mmoja anathubutu kuwa na mawazo ya ukaidi, na hivyo, kwa mujibu wa kiini cha amri za utawala Wangu, ulimwengu mzima umedhibitiwa vizuri na kwa utaratibu mzuri: Hakuna usumbufu umewahi kutokea, wala ulimwengu haujawahi kugawanyika. Ninaruka kwa kupaa juu ya nyota, na jua linapotoa miali yake, Ninalizuia joto la miali hiyo, Nikituma chembe kubwa za theluji kiwango cha manyoya ya bata bukini yakielea kwenda chini kutoka katika mikono Yangu. Hata hivyo, Ninapobadili mawazo Yangu, theluji yote inayeyuka na kuwa mto, na papo hapo, majira ya kuchipua yameibuka kila mahali chini ya anga na zamaradi ya kijani imeyageuza mazingira yote juu ya dunia. Mimi Naenda kuzunguka juu ya anga, na mara moja, nchi nzima imefunikwa katika giza “usiku” tititi kwa sababu ya umbo Langu: Bila ya onyo, “usiku” umewadia, na duniani kote ni giza mpaka hakuna anayeweza kuona mkono ulio mbele ya uso wake. Na kutoweka kwa mwanga, mwanadamu anachukua fursa ya kuanza uharibifu wa wenyewe kwa wenyewe, kunyakua na kuporana wenyewe. Mataifa ya dunia, kuingia katika hali ya mafarakano ya vurugu, yanaingia katika hali ya ghasia yenye matope, mpaka nafasi ambayo hawawezi kupata ukombozi. Wanadamu wanapambana katika machungu makubwa ya maumivu, kulia kwa uchungu katikati ya mateso, kuanza kuomboleza kwa hali ya kuhurumika katika mateso yao, wakitamani mwanga urejee kati yao kwa mara nyingine tena na hivyo kumaliza siku za giza na kurejesha uzima uliokuwepo. Lakini Mimi kwa muda mrefu Nimemwacha mwanadamu kwa kupapasa mkono wa vazi Langu, kamwe tena Nisimwonee huruma kwa sababu ya makosa ya dunia: Kwa muda mrefu Mimi nimechukizwa na kuwakataa watu wa dunia nzima, kufumba macho Yangu kwa hali duniani, kugeuza uso Wangu mbali na kila hatua ya mwanadamu, kila ishara zake, na kuacha kufurahiakutoridhishwa na uana wake na kutokua na hatia kwake. Mimi Nimeanza mpango mwingine wa kufanya dunia upya, ili dunia hii mpya iweze kupata kuzaliwa upya mapema na isizame tena. Miongoni mwa binadamu, mataifa mangapi ya kigeni yanasubiri Niyaweke kwenye haki, makosa mangapi ili Nije mwenyewe kuyazuia yasitendeke, ni vumbi kiasi gani ndio Mimi nije kufagia, ni siri ngapi za kufunuliwa Nami: binadamu wote wananingoja, na wanatamani kuja Kwangu.

Duniani, Mimi ni Mungu wa vitendo Mwenyewe katika mioyo ya watu; mbinguni, Mimi Ndiye

Mkuu wa viumbe vyote. Nimepanda milima na kuvuka mito, na Nimeingia na kutoka katikati ya binadamu. Nani anathubutu kwa uwazi kumpinga Mungu wa vitendo Mwenyewe? Nani anathubutu kutoka kati ya ukuu wa Mwenyezi? Nani anayethubutu kudai kuwa Mimi, bila shaka, Niko mbinguni? Tena, nani ambaye anathubutu kudai kuwa Mimi, bila kukosea, Niko duniani? Hakuna binadamu kati ya wote anayeweza kujieleza kwa ufasaha na undani mahali ambapo Mimi Naishi. Inawezekana kuwa kwamba, wakati Mimi niko mbinguni, Mimi ni Mungu Mwenyewe asiye wa kawaida? Inawezekana kuwa kwamba, wakati Mimi niko hapa duniani, Ninakuwa Mungu wa vitendo Mwenyewe? Kwamba Mimi ni Mtawala wa viumbe vyote, au kwamba Mimi ninapitia mateso ya ulimwengu wa mwanadamu—hakika hivi haviwezi kuamua iwapo Mimi ni Mungu wa vitendo Mwenyewe? Kama mwanadamu anadhani hivyo^[a], si yeye ni mpumbavu asiye na matumaini ya kubadilika? Mimi niko mbinguni; Mimi pia Niko duniani; Niko miongoni mwa mambo idadi kubwa ya viumbe, na pia katikati ya idadi kubwa ya watu. Mwanadamu anaweza kunigusa kila siku; zaidi ya hayo, anaweza kuniona kila siku. Kulingana na binadamu, Mimi huonekana kuwa wakati mwingine Nimejificha na wakati mwingine Naonekana; Mimi kwa kweli nipo, lakini pia naonekana kutokuwepo. Ndani Mwangu kuna siri kubwa sana zisizoweza kufahamika na binadamu. Ni kana kwamba watu wote wananitazama kwa njia ya hadubini ili kugundua siri hata zaidi ndani Mwangu, wakiwa na matumaini ya kuondoa hisia za wasiwasi katika nyoyo zao. Lakini hata watumie darubini ya nguvu kiviipi, binadamu watawezaje kuziweka wazi siri zilizo ndani Mwangu?

Wakati watu Wangu, kupitia kwa kazi Yangu, wanatukuzwa pamoja na Mimi, wakati huo maficho ya joka kubwa jekundu yatafichuliwa, matope yote na uchafu kufagiliwa mbali, na maji machafu, yaliyokusanyika kwa miaka mingi, kukaushwa na moto Wangu unaochoma, yasikuwepo tena. Hapo joka kubwa jekundu litaangamia katika ziwa la moto wa jehanamu. Je, kweli unayo nia ya kusalia chini ya ulinzi Wangu ili usinyakuliwe na joka? Je, kweli unachukia mbinu yake ya udanganyifu? Nani ambaye anaweza kuwa shahidi Wangu wa dhati? Kwa ajili ya jina Langu, kwa ajili ya Roho Wangu, na kwa sababu ya mpango Wangu mzima wa usimamizi, ni nani anayeweza kutoa nguvu zake zote? Leo, wakati ambao ufalme upo katika ulimwengu wa wanadamu, ni wakati ambao Nimekuja binafsi miongoni mwa binadamu. Kama haingekuwa hivyo, je, kuna yeyote ambaye anaweza kujitokeza aende kwenye uwanja wa vita kwa niaba Yangu bila hofu yoyote? Ndipo ufalme uweze kuchukua mkondo, ili moyo Wangu uweze kuridhika, na tena, ili siku Yangu iweze kuja, ili wakati uweze kuja ambapo mambo mengiya uumbaji yamezaliwa upya na kukua kwa wingi, ili kwamba mwanadamu aweze kuokolewa kutoka kwenye bahari ya mateso, ili siku inayofuata iweze kuja, na ili iwe ni ya ajabu, yenye kutoa maua na kushamiri, na tena, ili starehe ya siku za usoni itimizwe, binadamu wote wanajitahidi kwa nguvu zao zote, bila kuwacha chochote katika kujitoa sadaka wenyewe kwa

ajili Yangu. Je, hii si ishara kwamba ushindi tayari ni Wangu, na alama ya kukamilika kwa mpango Wangu?

Wanadamu wanavyozidi kukaa katika siku za mwisho, ndivyo watakavyozidi kuhisi utupu wa dunia na ndivyo watakavyopungukiwa na ujasiri wa jinsi ya kuishi. Kwa sababu hii, watu wasiohesabika wamekufa katika hali ya kuvunja matumaini, wengine wengi wamevunjwa matumaini katika jitihada zao, na wengine wengi kuteseka wenyewe kuwa kunyanyaswa katika mikono ya shetani. Mimi Nimewaokoa watu wengi, Nimewapa wengi msaada, na mara nyingi, wakati binadamu wamepoteza mwanga, Mimi Nimewaongoza kurudi katika nafasi ya mwanga, ili wapate kunijua wakiwa kwenye mwanga, na kunifurahia katika furaha. Kwa sababu ya ujio wa mwanga Wangu, kuabudu hukuzwa katika mioyo ya watu wanaokaa katika ufalme Wangu, kwa maana Mimi ni Mungu wa kupendwa na binadamu, Mungu ambaye binadamu unajishika katika hali ya upendo, na mwanadamu anajazwa na maono ya kudumu ya umbo Langu. Hata hivyo, baada ya yote, hakuna mtu anayeelewa ikiwa hii ni kazi ya Roho au ni kazi ya mwili. Itawachukua watu maisha yote kupitia jambo hili moja. Wanadamu hawajawahi kunichukia ndani ya vina vya mioyo yao; badala yake, wananishikilia katika vina vya roho zao. Hekima yangu inaibua upendezewaji wake, maajabu Ninayotenda ni ukuu machoni pake, maneno Yangu yanastaajabisha akili yake, na bado yeye ana mapenzi tele kwayo. Uhalisi Wangu unawaacha wanadamu wasijue la kufanya, wakipigwa na butwaa na kukanganyikiwa, na bado wako tayari kuukubali. Je, hiki si kipimo cha mwanadamu jinsi alivyo hasa?

Machi 13, 1992

Tanbihi:

a. Maandiko ya asilia yanasema “Katika hali hii.”

Sura ya 16

Kuna mengi ambayo Natamani kumwambia mwanadamu, mambo mengi sana ambayo lazima Nimwambie. Lakini uwezo wa mwanadamu wa kukubali una upungufu mwingi: Hana uwezo wa kuyaelewa kabisa maneno Yangu kulingana na kile Ninachokitoa, na anaelewa kipengele kimoja tu lakini haelewi vingine. Lakini Simwangamizi mwanadamu kwa ajili ya ukosefu wake wa nguvu, wala Siudhiki na udhaifu wake. Naifanya kazi Yangu tu, na kuongea jinsi ambavyo Nimefanya, hata kama mwanadamu haelewi matakwa Yangu; siku itakapokuja, watu watanijua ndani kabisa ya nyoyo zao, na watanikumbuka katika mawazo yao. Nitakapoondoka duniani ndipo haswa Nitakapopanda kwa kiti cha enzi katika moyo wa binadamu, yaani, itakuwa wakati watu wote watanijua Mimi. Hivyo pia, itakuwa wakati wana Wangu na watu watatawala dunia. Wale ambao wananjua Mimi bila shaka watakuwa nguzo za

ufalme Wangu, na wao peke yao ndio watastahiki kutawala na kuwa na mamlaka katika ufalme Wangu. Wote ambao wananijua Mimi wana nafsi Yangu, na wana uwezo wa kuishi kwa kunidhihirisha miongoni mwa watu wote. Sijali mwanadamu ananijua Mimi kwa kiwango gani: Hakuna yeyote anayeweza kuzuia kazi Yangu kwa njia yoyote, na mwanadamu hawezi kunipa usaidizi wowote wala kunifanyia lolote. Mwanadamu anaweza tu kufuata mwongozo Wangu katika mwangaza Wangu, na kutafuta matakwa Yangu kwenye mwangaza huu. Leo, watu wana sifa zinazostahili, na wanaamini wanaweza kutembea kwa maringo mbele Yangu, na kucheka na kufanya mzaha na Mimi bila kizuizi hata kidogo, na kunihutubia Mimi kama tuko sawa. Bado mwanadamu hanijui Mimi, bado anaamini kuwa kiasili sisi kadri tuko sawa, kuwa sisi sote ni nyama na damu, na sote tunaishi katika dunia ya binadamu. Uchaji wake Kwangu ni mdogo sana; ananiheshimu Mimi anapokuwa mbele Yangu, lakini hawezi kunihudumia Mimi mbele ya Roho. Ni kama, kwa mwanadamu, Roho hayupo kabisa. Kwa hivyo, hakuna mwanadamu ashawahi kumjua Roho; katika kupata mwili Kwangu, watu huona tu mwili wa nyama na damu, na hawamtambui Roho wa Mungu. Matakwa Yangu yanaweza kutimizwa kwa njia kama hii? Watu ni mabingwa wa kunihadaa Mimi; wanaonekana kama ambao wamepewa mafunzo maalum na Shetani ili kunihadaa Mimi. Lakini Shetani bado hanibabaishi Mimi. Bado Nitatumia hekima Yangu kuwashinda wanadamu wote na kumshinda ambaye anawapotosha wanadamu wote, ili ufalme Wangu uanzishwe duniani.

Miongoni mwa binadamu, kuna wale ambao wamejaribu kujua ukubwa wa nyota, au upana wa mbingu. Lakini utafiti wao haujawahi kuweza kuzaa matunda, na hawana hiari ila tu kuinamisha vichwa vyao kwa masikitiko na kukubali kushindwa. Nikiwaangalia watu wote na kuchunguza uwezo wa mwanadamu katika kushindwa kwake, Sioni yeyote yule ambaye ameniamini kabisa, hakuna ambaye ananitii Mimi na kujinyenyekeza Kwangu. Matarajio ya wanadamu ni yasiyo ya kawaida kweli! Wakati yote yalikuwa yamefunikwa na kiza, miongoni mwa wanadamu Nilianza kuonja uchungu wa dunia. Roho Wangu husafiri kote duniani na kuangalia ndani ya nyoyo za watu wote, na bado pia, Mimi huwashinda wanadamu katika mwili wangu wa nyama. Mwanadamu huwa hanioni Mimi, kwa kuwa yeye ni kipofu; mwanadamu hanijui Mimi, kwani amekuwa hana hisia; mwanadamu hunipinga Mimi, kwa kuwa yeye si mtiifu; mwanadamu huja kusujudu mbele Yangu, kwa kuwa ameshindwa na Mimi; mwanadamu huja kunipenda Mimi, kwa kuwa Nastahili kiasili kupata upendo wa mwanadamu; mwanadamu huishi kulingana na Mimi na kunidhihirisha Mimi, kwa sababu nguvu Zangu na hekima Yangu humfanya apendeze nafsi Yangu. Nina nafasi katika moyo wa mwanadamu, lakini kamwe Sijawahi kupokea upendo wa mwanadamu Kwangu katika roho yake. Kwa kweli, kuna mambo katika roho ya mwanadamu anayoyapenda kuliko yote mengine, lakini Mimi si mojawapo wa mambo hayo, na kwa hivyo upendo wa mwanadamu ni kama kiputo cha sabuni: Upepo

unapovuma, hukipasua na kinaenda, kisiwahi kuonekana tena. Mtazamo Wangu kuhusu mwanadamu siku zote umekuwa thabiti na usiobadilika. Kuna yeyote kati ya wanadamu, ambaye angeweza kufanya vivyo hivyo? Machoni pa mwanadamu, Mimi sigusiki wala Mimi sionekani mithili ya hewa, na kwa sababu hii, idadi kubwa ya watu hutafuta tu katika anga isiyokuwa na mipaka, au juu ya bahari ambayo si tulivu, au juu ya ziwa tulivu, au miongoni mwa maandiko na mafundisho matupu. Hakuna mtu hata mmoja anayejua kiini cha binadamu, sembuse yeyote anayeweza kusema chochote kuhusu fumbo lililo ndani Yangu, na kwa hivyo huwa Simtaki mwanadamu afikie viwango vya juu zaidi ambavyo yeye hudhani Nahitaji kutoka kwake.

Ndani ya maneno Yangu, milima hupinduliwa, maji hutiririka kinyumenyume, mwanadamu huwa mtiifu, na maziwa huanza kutiririka bila kusita. Ingawa bahari isiyo tulivu huenda kwa hasira kuelekea mbinguni, ndani ya maneno Yangu bahari za aina hii hutulia kama upande wa juu wa ziwa. Kwa kupunga mkono Wangu kidogo tu, upepo mkali kabisa hutokomea na kutoka Kwangu mara moja, na ulimwengu wa mwanadamu hurejesha utulivu wake mara moja. Lakini Ninapotoa ghadhabu Yangu, milima hutenganishwa mara moja, ardhi huanza kutetemeka mara moja, maji hukauka mara moja, na mwanadamu huzingirwa na maafa mara moja. Kwa ajili ya ghadhabu Yangu, huwa Mimi sisikilizi vilio vya mwanadamu, huwa sitoi msaada ili kujibu vilio vyake, kwani hasira Yangu inapanda. Ninapokuwa miongoni mwa mbingu, nyota hazijawahi kutishiwa na kuwepo Kwangu kamwe. Bali, huwa zinaweka nyoyo zao katika kunifanyia kazi Mimi, na kwa hivyo, Mimi huzipa mwangaza zaidi na kuzifanya zing'are zaidi, ili zipate utukufu zaidi kwa ajili Yangu. Kadri mbingu inavyong'aa zaidi, ndivyo dunia chini yake inazidi kuwa na giza; watu wengi sana hulalamika kuwa mipango Yangu huwa haifai, wengi wameniacha kuunda ufalme wao wenyewe, ambao wanautumia kunisaliti, na kubadili hali ya giza. Ila nani ameweza kutimiza hili kwa azma yao? Ni nani ametimiza hili kwa azimio lake? Nani anaweza kubadili yale ambayo yamepangwa na mkono Wangu? Wakati majira ya machipuko yanaenea kwenye ardhi, Mimi hupeleka mwangaza kwa siri na kimya ulimwenguni, ili, duniani, mwanadamu awe na hisia ya ghafla ya usafi hewani. Hata hivyo, wakati huo huwa Ninafunika macho ya mwanadamu, ili aone tu ukungu ukiwa umefunika ardhi, na watu na vitu vyote havibainiki. Watu kupumua tu kwa masikitiko. Mbona mwangaza uling'aa kwa muda mdogo tu? Kwa nini Mungu humpa binadamu ukungu na utusitusi tu? Huku watu wakikata tamaa, ukungu hupotea mara moja, lakini wanapooa dalili ya mwangaza, Mimi huachilia mbubujiko wa mvua juu yao, na viwambo vyao vya masikio vinavunjwa kwa ajili ya mvua na radi wanapolala. Huku wakiwa na hofu, hawana wakati wa kujikinga, na hugubikwa na mvua kubwa. Papo hapo, yote yaliyo chini ya mbingu hufagiliwa katika ghadhabu Yangu yenye hasira. Watu hawalalamiki tena kuhusu mwanzo wa mvua kubwa, na ndani yao wote, uchaji huzaliwa. Kwa sababu ya uvamizi huu wa ghafla wa mvua, idadi kubwa ya watu wanazama ndani ya maji yanayonyesha kutoka mbinguni,

na kuwa maiti ndani ya maji. Naangalia dunia nzima na kuona kuwa wengi wanazinduka, kuwa wengi wanatubu, kuwa wengi wanatafuta chanzo cha maji ndani ya mashua ndogo, kuwa wengi wananisujudu Mimi ili kuomba msamaha Wangu, kuwa wengi wameona mwangaza, kuwa wengi wameona uso Wangu, kuwa wengi wana ujasiri wa kuishi, na kuwa ulimwengu mzima umebadilishwa. Kufuatia mbubujiko huu mkubwa wa mvua, vitu vyote vimerudi kuwa jinsi vilivyokuwa katika akili Yangu, na haviasi tena. Kabla ya muda mrefu, ardhi yote imejaa sauti za vicheko, na kila mahali duniani kuna hali ya sifa, na hakuna popote ambapo hapana utukufu Wangu. Hekima Yangu iko kote duniani, na katika ulimwengu mzima. Miongoni mwa vitu vyote, kuna matunda ya hekima Yangu, miongoni mwa watu wote, kumejaa kazi bora zaidi za hekima Yangu; kila kitu ni kama mambo yote katika ufalme Wangu, na watu wote wanakaa kwa mapumziko chini ya mbingu Zangu kama kondoo kwenye uwanja Wangu wa malisho. Nasonga juu ya wanadamu wote na Natazama kila mahali. Hakuna kinachokaa kizee kamwe, na hakuna mtu ambaye yuko kama alivyokuwa. Ninapumzika katika kiti cha enzi, Naegemea juu ya ulimwengu mzima, na Nimeridhika kikamilifu, kwani kila kitu kimerejesha utakatifu wake, na Ninaweza kukaa kwa amani ndani ya Zayuni tena, na watu duniani wanaweza kuishi maisha tulivu na ya kuridhisha chini ya mwongozo Wangu. Watu wote wanasimamia kila kitu mikononi Mwangu, watu wote wamerejesha akili zao za awali na mwonekano wao wa kiasili; hawafunikwi tena na vumbi, lakini, ndani ya ufalme Wangu, ni safi kama lulu, kila mmoja akiwa na uso kama vile wa yule mtakatifu aliye ndani ya moyo wa binadamu, kwani ufalme Wangu umeimarishwa miongoni mwa binadamu.

Machi 14, 1992

Sura ya 17

Sauti Yangu inatoka kama radi, ikitia nuru roboduara zote nne na dunia nzima, na katikati ya radi na umeme, binadamu wanaangushwa chini. Hakuna mwanadamu aliyewahi kusimama imara katikati ya radi na umeme: Wanadamu wengi wanaogopa sana kuja kwa mwangaza Wangu na hawajui cha kufanya. Wakati mwangaza hafifu unaanza kuonekana Mashariki, watu wengi, wakiongozwa na huu mng'ao dhaifu, wanaamshwa mara moja kutoka kwa njozi zao. Lakini, hakuna aliyewahi kutambua kwamba siku imewadia mwangaza Wangu unaposhuka duniani. Wanadamu wengi wanashtuliwa na ujio wa ghafla wa mwangaza; baadhi yao, kwa macho ya kuvutiwa ya dadisi, wanaangalia mwendo wa mwangaza na kutoka upande upi unasongea; ama wengine wanasimama tayari wakitazama mwangaza, ili waweze kuelewa wazi zaidi palipotoka mwangaza. Iwe ilivyo, kuna yeyote aliyewahi kugundua thamani ya mwangaza wa leo? Kuna yeyote aliyewahi kufahamu ajabu ya mwangaza huu? Wanadamu wengi wamechanganyikiwa tu; wamejeruhiwa machoni na kutupwa chini matopeni na mwangaza. Mtu

anaweza kusema kwamba, chini ya mwangaza huu usiokuwa na ufasili, dunia imefunikwa na vurugu, ikifanya mtazamo wa kusikitisha usiovumilika ambao, ukichunguzwa kwa kina, unamtesa mtu na huzuni nyingi. Kutoka hapa, mtu anaelewa kwamba, wakati mwangaza una nguvu kabisa, hali ya dunia itakuwa na uwezo mdogo zaidi wa kumruhusu mwanadamu kusimama mbele Yangu. Binadamu uko katika mng'ao wa mwangaza; tena, binadamu uko katika wokovu wa mwangaza lakini kwa wakati huo huo pia chini ya majeraha yanayotokana na mwangaza: Kuna yeyote asiye chini ya mapigo yanayoua ya mwangaza? Kuna yeyote anayeweza kutoroka kuchoma kwa mwangaza? Nimetembea kote duniani, kutawanya mbegu za Roho Wangu, ili binadamu wote duniani kwa sababu hii wataongozwa nami. Kutoka kwa urefu wa juu wa mbingu, Naangalia chini kwa dunia yote, Nikitazama matukio ya ajabu na yasiyo ya kawaida ya viumbe wa dunia. Sehemu ya juu ya bahari inaonekana kuteswa na mshtuko wa tetemeko la ardhi: Ndege wa bahari wanaruka hapa na pale, wakitafuta samaki wa kumeza. Wakati huo huo, hii haijulikani chini ya bahari, ambayo hali ya sehemu ya juu haiwezi kabisa kuzindua fahamu, kwa sababu chini ya bahari kutulia kama mbingu ya tatu: Hapa viumbe vilivyo hai vikubwa na vidogo vinaishi pamoja kwa amani, bila kushiriki katika “migogoro ya mdomo na ulimi” hata mara moja. Miongoni mwa matukio ya ajabu na ya kichekesho, binadamu ndio unaoona ni vigumu sana kuniridhisha. Nafasi Niliyompa mwanadamu ni ya juu sana, na hivyo basi tamaa yake ni kubwa mno, na ndani ya macho yake daima kuna kiwango cha kutotii. Katika hali Yangu ya kumfundisha nidhamu mwanadamu, ndani ya hukumu Yangu kwake, kumekuwa na mengi yenye maumivu, mengi yaliyo na wema, lakini kwa mambo haya mwanadamu hana habari hata kidogo. Sijawahi kumshughulikia mwanadamu yeyote kwa ukali: Nimepeana tu marekebisho mwafaka, wakati mwanadamu hajatii, na tu, wakati mwanadamu amekuwa mdhaifu, Nimetoa msaada mwafaka. Lakini, wakati binadamu unaendelea kujitenga nami na zaidi ya hayo unatumia mipango danganyifu ya Shetani kuasi dhidi Yangu, Nitamwangamiza mwanadamu mara moja, Nikiwaacha wanadamu bila nafasi ya kufanya maonyesho makuu ya ujuzi wao mbele Yangu, ili wasiweze tena kujigamba na madoido na hali, wakionea wengine, duniani.

Natumia mamlaka Yangu duniani, Nikidhihirisha kazi Yangu yote. Yote yaliyo katika kazi Yangu yanajitokeza duniani; mwanadamu hajawahi, duniani, kuweza kuufahamu mwendo Wangu mbinguni, wala kutafakari kabisa mizunguko na njia za Roho Wangu. Wanadamu wengi wanaelewa tu maelezo madogo yaliyo nje ya roho, bila kuweza kuelewa hali halisi ya roho. Matakwa Yangu kwa binadamu hayatoki kwa Mimi wa mbinguni Nisiye dhahiri, ama kwa Mimi wa dunia Nisiyekadiriwa: Natoa matakwa ya kufaa kulingana na kimo cha mwanadamu. Sijawahi kumweka yeyote kwa matatizo, wala Sijawahi “kukamua damu ya mtu yeyote” ili kujiridhisha—inawezakana kwamba matakwa Yangu kuzuiliwa na masharti haya pekee? Kwa

viumbe lukuki duniani, ni yupi asiyetii tabia za maneno yaliyo mdomoni Mwangu? Ni yupi kati ya viumbe hawa, wanaokuja mbele Yangu, hajachomwa kabisa kupitia maneno Yangu na moto Wangu unaochoma? Ni yupi kati ya viumbe hawa anayethubutu kujigamba mbele Yangu? Ni yupi kati ya viumbe hawa hainami mbele Yangu? Mimi ni Mungu anayelazimisha tu ukimya kwa viumbe? Kwa mambo lukuki katika uumbaji, Nachagua yale yanaoridhisha nia Yangu; kwa wanadamu lukuki, Nawachagua wale wanaotunza roho Yangu. Nachagua bora zaidi kwa nyota zote, hivyo Naongeza mwangaza hafifu kwa ufalme Wangu. Natembea duniani, Nikitawanya harufu Yangu nzuri kila mahali, nami Naacha umbo Langu kila mahali. Kila pahali panatingika kwa mvumo wa sauti Yangu. Watu kila mahali wanadumu kwa hamu ya mambo waliyozea ya urembo wa mandhari ya jana, kwani binadamu wote wanakumbuka siku za nyuma ...

Binadamu wote wanatamani kuona uso Wangu, lakini Nishukapo Mwenyewe duniani, wote wanakirihishwa na ujio Wangu, wote wanaufukuza mwangaza usije, kana kwamba Mimi ni adui ya mwanadamu mbinguni. Mwanadamu ananisalimu na mwangaza wa kujikinga machoni mwake, na daima anabaki katika tahadhari, akihofia sana kwamba Naweza kuwa na mipango mingine kwake. Kwa sababu binadamu wananiona kama rafiki asiyejulikana, wanahisi kwamba Nina nia ya kuwaua bila kujali. Katika macho ya mwanadamu, Mimi ni adui wa mauti. Baada ya kuonja joto Langu katikati ya msiba, mwanadamu hata hivyo bado hafahamu pendo Langu, na bado ameamua kunifukuza na kunikaidi. Mbali na kujinufaisha na yeye kuwa katika hali hii ili kuchukua hatua dhidi yake, Namfunika mwanadamu na joto la kumbatio, Najaza mdomo wake na utamu, na kuweka chakula anachohitaji tumboni mwake. Lakini, wakati hasira Yangu ya ghadhabu inapotingiza milima na mito, Sitamtawaza mwanadamu aina mbalimbali za msaada, kwa sababu ya woga wake. Wakati huu, Nitakuwa na ghadhabu, Nikiwanyima viumbe hai fursa ya kutubu na, kuachana na matumaini Yangu yote kwa mwanadamu, Nitatoa adhabu anayostahili sana. Wakati huu, radi na umeme vinang'aa ghafla na kunguruma, kama mawimbi ya bahari yakisonga kwa hasira, kama milima makumi ya maelfu ikigonga chini. Kwa ajili ya uasi wake, mwanadamu anaangushwa na radi na umeme, viumbe wengine wanafutwa katika milipuko ya radi na umeme, ulimwengu mzima unazorota ghafla katika machafuko, na uumbaji huwezi kupata pumzi muhimu ya uhai. Majeshi lukuki ya binadamu hayawezi kutoroka kishindo cha radi, katikati ya nuru ya ghafla ya umeme, wanadamu, makundi mengi sana, wanaanguka ndani ya mto unaobubujika haraka, kutokomezwa na mafuriko yanayotiririka chini kutoka milima. Ghafla, panakutana dunia ya “wanadamu” badala ya hatima ya binadamu. Maiti wanasongasonga juu ya bahari. Binadamu wote wanaenda mbali nami kwa sababu ya ghadhabu Yangu, kwani mwanadamu ametenda dhambi dhidi ya kiini cha Roho Wangu, uasi wake umenikosea Mimi. Lakini, mahali ambapo hakuna maji, wanadamu wengine bado wanafurahia, wakicheka na kuimba, ahadi ambazo Nimewapa.

Binadamu wote wanapotulia, Natoa kimulimuli cha mwangaza mbele ya macho yao. Hapo, wanadamu wanakuwa na uwazi wa akili na uangavu wa jicho, na wanakoma kuwa na nia ya kukimya; hivyo, hisia ya kiroho inakusanywa ndani ya mioyo yao mara moja. Wakati huu, binadamu wote wanafufuka. Wakiweka kando malalamiko yao, wanadamu wote wanakuja mbele Yangu, baada ya kushinda nafasi nyingine ya kusalimika kupitia maneno Ninayotangaza. Hii ni kwa sababu wanadamu wote wanataka kuishi duniani. Lakini nani miongoni mwao amewahi kuwa na nia ya kuishi kwa ajili Yangu? Nani miongoni mwao amewahi kufichua mambo mazuri ndani yake kunipa furaha? Nani miongoni mwao amewahi kugundua harufu ya kuvutia Kwangu? Wanadamu wote ni vitu hafifu na visivyotakaswa: Nje, wanaonekana kuangaza macho, lakini kwa nafsi zao muhimu hawanipendi kwa dhati, kwa sababu ndani ya nafasi ya kina cha moyo wa binadamu hakujawahi kuwa hata na kiasi kidogo cha Mimi. Mwanadamu anakosa sana: Kumlinganisha nami Mwenyewe, ingeonekana kwamba tuko mbali sana kama dunia kutoka kwa mbingu. Lakini, hata hivyo, Simshambulii mwanadamu katika sehemu zake dhaifu na zenye kasoro, wala Simchekei kudharau upungufu wake. Mikono Yangu imekuwa kazini duniani kwa maelfu ya miaka, na muda huo wote, macho Yangu yamelinda binadamu wote. Bado, Sijawahi kuchukulia mzaha maisha ya binadamu hata mmoja kana kwamba ni kitu cha kuchezea. Nachunguza machungu mwanadamu amechukua na kuelewa bei ambayo amelipa. Anaposimama mbele Yangu, Sitamani kumpata mwanadamu kwa kumshtua kwa nia ya kumwadibu, wala kumtakia na kutawaza kwake vitu visivyohitajika. Badala yake, wakati huu wote nimemchunga mwanadamu, na kumpa mwanadamu, wakati huu wote. Hivyo basi, yote anayofurahia mwanadamu ni neema Yangu, yote ni fadhila inayotoka kwa mkono Wangu. Kwa sababu Niko duniani, mwanadamu hajawahi lazimika kuteseka mateso ya njaa. Badala yake, Namruhusu mwanadamu kupokea kutoka mikono Yangu mambo ambayo anaweza kufurahia, na kumruhusu mwanadamu kuishi ndani ya baraka Zangu. Je, wanadamu wote hawaishi chini ya kuadibu Kwangu? Kama tu jinsi kuna mengi ndani ya vina vya milima, na vitu vingi vya kufurahia ndani ya maji, je, watu wanaoishi ndani ya maneno Yangu leo wanavyo, hata zaidi, chakula wanachopenda na kuonja? Niko duniani, na mwanadamu anafurahia baraka Zangu duniani. Niachapo dunia nyuma, ambapo ndipo pia kazi Yangu itafika ukamilishaji wake, wakati huo, wanadamu hawatapata tena hisani yoyote kutoka Kwangu kwa sababu ya udhaifu wao.

Machi 16, 1992

Sura ya 18

Katika mwako wa umeme, kila mnyama hufichuliwa katika hali yake halisi. Hivyo pia, kama wameangaziwa na mwanga Wangu, mwanadamu amepata tena utakatifu aliokuwa nao wakati mmoja. Eh, dunia potovu ya zamani! Mwishowe, imeanguka na kutumbukia ndani ya

maji machafu na, imezama chini ya maji, na kuyeyuka na kuwa tope! Ah, ya kwamba binadamu wote Niliouumba hatimaye umerudiwa na uhai tena katika mwanga, kupata msingi wa kuwepo, na kuacha kupambana katika tope! Ah, Mambo mengi ya uumbaji Ninayoyashikilia mikononi Mwangu! Wanawezaje, kukosa kufanywa upya, kupitia maneno Yangu? Wanawezaje, katika mwanga, kukosa kuendeleza kazi zao? Dunia si kimya cha mauti na nyamavu tena, mbingu si ya ukiwa na yenye huzuni tena. Mbingu na nchi, bila kutenganishwa na utupu tena, zimeungana kama kitu kimoja, kamwe kutotenganishwa tena. Katika wakati huu wa shangwe, wakati huu wa nderemo, haki Yangu na utakatifu Wangu umeenea katika kila pembe ya ulimwengu, na binadamu wote wanavisifu bila kikomo. Miji yote ya mbingu inacheka kwa furaha, na falme zote za nchi zinacheza kwa shangwe. Ni nani wakati huu ambaye haonyeshi furaha? Na ni nani wakati huu ambaye halii? Nchi katika hali yake ya asili ni miliki ya mbingu, na mbingu imeungana na nchi. Mwanadamu ni ugwe unaounganisha mbingu na nchi, na kwa sababu ya utakatifu wa mwanadamu, kwa ajili ya kufanywa upya kwa mwanadamu, mbingu haijafichwa tena kutoka kwa nchi, na nchi haiko kimya tena kwa mbingu. Nyuso za binadamu zimezingirwa na tabasamu za shukurani, na nyoyo zao zinadondokwa na utamu usiokuwa na kifani. Mwanadamu hagombani na mwanadamu, wala binadamu kupigana wenyewe kwa wenyewe. Kunao wale ambao, katika mwanga Wangu, hawaishi kwa furaha na wenzao? Kunao wale ambao, katika siku Yangu, hulifedhehesha jina Langu? Watu wote huelekeza macho yao ya heshima Kwangu, na wao hunililia kwa siri katika nyoyo zao. Nimechunguza kila kitendo cha binadamu: Miongoni mwa wanadamu waliotakaswa, hakuna yeyote aliye mkaidi Kwangu, hakuna anayenielekezea hukumu. Binadamu wote umejawa na tabia Yangu. Kila mtu anakuja kunijua, ananijongelea, na ananiabudu. Msimamo wangu ni mmoja katika roho ya mwanadamu, Nimetukuzwa kwa kiwango cha juu zaidi kwa macho ya mwanadamu, na hububujika katika damu ya mishipa yake. Nderemo za furaha katika nyoyo za wanadamu huenea kila sehemu ya uso wa nchi, hewa ni ya kuchangamsha na bichi, ukungu mzito huitandai ardhi tena, na mwangaza wa jua huvutia.

Sasa, ona ufalme Wangu, ambamo Mimi ni mfalme juu ya vyote, na Ninamotawala juu ya vyote. Tangu mwanzo wa uumbaji hadi sasa, wana wangu, wakiongozwa na Mimi, wameyapitia matatizo mengi sana ya maisha, dhuluma nyingi za ulimwengu, mageuko mengi sana ya ulimwengu wa binadamu, lakini sasa huishi katika nuru Yangu. Je, ni nani asiyelia kwa ajili ya dhuluma za jana? Je, ni nani ambaye hatokwi na machozi juu ya dhiki za kuifikia leo? Na tena, kuna wowote ambao hawaichukui fursa hii kujitolea kwa dhati kwa ajili Yangu? Je, kuna wowote ambao hawachukui fursa hii kuonyesha uchu unaochipuka mioyoni mwao? Je, kuna wowote ambao, wakati huu, hawaongei juu ya yale waliyoyapitia? Wakati huu, binadamu wote wanaziweka wakfu sehemu zao zilizo bora zaidi kwa ajili Yangu. Ni wangapi wanateseka na

majuto kwa upumbavu wa giza wa jana, ni wangapi wanajichukia kwa sababu ya malengo ya jana. Binadamu wote wamepata kujijua, wote wameona matendo ya Shetani na maajabu Yangu, ndani ya nyoyo zao, sasa kuna nafasi kwa ajili Yangu. Sitakumbana tena na chuki na kukataliwa miongoni mwa wanadamu, kwani kazi Yangu kubwa imekwisha tekelezwa, na haizuiliwi tena. Leo, miongoni mwa wana Wangu, kunao wowote ambao hawajatafakari kwa niaba yao wenyewe? Kunao wowote ambao hawadhukuru zaidi kwa ajili ya njia ambazo kwazo kazi Yangu ilifanywa? Kunao wowote ambao wamejitolea kwa kweli kwa ajili Yangu? Uchafu ulio ndani ya mioyo yenu umepungua? Ama umeongezeka? Iwapo sehemu chafu katika nyoyo zenu hazijapungua, na wala hazijaongezeka, basi bila shaka Nitawatupa watu kama hao. Wale Ninaowataka ni watu watakatifu wanaoupendeza moyo Wangu, sio ibilisi wachafu wanaoniasi. Hata ingawa matakwa Yangu kwa binadamu si ya juu, ulimwengu wa ndani wa nyoyo za watu una changamano kiasi kwamba binadamu hauwezi kuafikiana na mapenzi Yangu bila kusita ama mara moja kutosheleza mahitaji Yangu. Wengi wa wanadamu wanaweka jitihada kisiri kwa matumaini ya kuweza kupata laurusu ya kuvishwa taji hatimaye. Idadi kubwa ya wanadamu wanajitahidi kwa nguvu zao zote, bila kuzembea hata kidogo, wakiogopa sana kutekwa nyara na Shetani tena. Hawathubutu tena kuwa na manung'uniko juu Yangu, lakini daima huonyesha utiifu wao Kwangu. Nimesikia maneno ya dhati yakinenwa na watu wengi, simulizi kutoka kwa watu wengi sana kuhusu matukio machungu ya mateso waliyopitia; Nimeona wengi sana, katika dhiki kubwa sana, wakinipa utiifu wao bila kukosa, na Nimewatazama wengi sana, wakitembea kwenye njia yenye mabonde, wakitafuta suluhisho. Katika hali hizi, hawajawahi kulalamika; hata wakati, wakishindwa kupata mwanga, walijipata kuwa wenye huzuni kidogo, hawajawahi kulalamika hata mara moja. Lakini pia Nimesikia watu wengi sana wakitoa mawazo yao bila woga kwa maapizo kutoka kwa vina vya nyoyo zao, wakiilaani Mbingu na kuishutumu nchi, na Nimeona, vilevile, watu wengi sana wakijiruhusu kukata tamaa katikati ya dhiki yao, wakijitupa mbali kama taka kwa jaa, halafu kufunikwa kwa uchafu na masizi. Nimesikia watu wengi sana wakigombana baina yao, kwa sababu mabadiliko katika cheo, pamoja na mabadiliko ya mwonekano wa nyuso zao yanayoandamana nayo, yamesababisha mabadiliko katika uhusiano wao na binadamu wenzao, hivi kwamba marafiki wanaacha kuwa marafiki na kuwa maadui, huku wakishambuliana kwa midomo. Wengi wa watu hutumia maneno Yangu kama risasi kutoka kwa bombomu, wakiwafyatulia wengine kwa ghafla, hadi ulimwengu wa waume umejawa kila mahali na makelele yanayoharibu kimya kitulivu. Kwa bahati nzuri, sasa ni leo; ama sivyo ni nani anayejua ni wangapi wangukuwa wamekufa kupitia kwa mfululizo usio na huruma wa moto huu wa bombomu.

Kufuatia maneno yanayotoka Kwangu, na kwenda sambamba na hali za binadamu wote, ufalme Wangu, hatua kwa hatua, hushuka duniani. Mwanadamu hahodhi tena fikira zenye

wasiwasi, ama “kuzingatia” mambo ya watu wengine, au “kutafakari” kwa niaba yao. Na hivyo, migogoro yenye ubishi duniani haipo tena, na, kufuatia kutolewa kwa maneno Yangu, ‘silaha’ mbali mbali za enzi ya sasa zimeondolewa. Binadamu hupata amani na binadamu, moyo wa binadamu hunururisha roho ya uwiano tena, hakuna yeyote mwenye mwelekeo wa kujikinga dhidi ya mashambulizi ya siri. Binadamu wote wamerudi katika hali ya kawaida na kuanza maisha mapya. Wakiishi katika mazingira mapya, idadi kubwa ya watu huangalia kandokando yao, wakiishi kana kwamba wameingia katika ulimwengu mpya kabisa, na kwa sababu ya hili, wanashindwa kubadilika mara moja katika mazingira yao ya sasa ama kuingia mara moja kwenye njia nyofu. Na kwa hivyo linakuwa ni jambo la “roho iko radhi, lakini mwili ni dhaifu” kwa kadiri binadamu unavyohusika. Ingawa Mimi, kama mtu, sijaonja machungu ya mashaka Mwenyewe, Nayajua yote ya kujulikana kuhusu upungufu wa mwanadamu. Ninayaelewa kwa undani mahitaji ya mtu, na uelewa Wangu wa udhaifu wake ni mtimilifu. Kwa sababu hii, Simfanyii mzaha binadamu kwa dosari zake; Mimi husimamia tu, kulingana na udhalimu wa mwanadamu, kipimo mwafaka cha ‘elimu,’ bora zaidi ili kumwezesha kila mtu kushika njia nyofu, ili kwamba binadamu waache kuwa mayatima wanaozurura na badala yake wawe watoto wachanga walio na makao. Hata hivyo, matendo Yangu yanaelekezwa na kanuni. Kama wanadamu hawataki kufurahia upeo wa furaha iliyo ndani Yangu, Ninaweza kukubaliana tu na kile ambacho mioyo yao inatamani kufanya na kuwatupa katika shimo lisilo na mwisho. Katika hatua hii, hakuna anayestahili kuyahodhi malalamiko moyoni mwake tena, ila wote wanapaswa kuona haki Yangu katika mipango ambayo Nimeifanya. Siulazimishi binadamu kunipenda Mimi, wala Sitampiga mwanadamu yeyote kwa kunipenda Mimi. Ndani Yangu ni uhuru kamili, ufunguliwaji kamili. Ingawa majaliwa ya mtu yamo mikononi Mwangu, Nimempa binadamu hiari ambayo haitegemei uongozi Wangu. Kwa njia hii, wanadamu hawatabuni njia za kuingia katika matatizo kwa sababu ya amri Zangu za kiutawala, bali, kwa kutegemea ukarimu Wangu, watajipatia ufunguliwaji. Na kwa hivyo watu wengi, bila kufungiwa katika kizuizi Kwangu, huenda kutafuta njia yao wenyewe ya kutoka, katika tendo la kupata ufunguliwaji.

Daima Mimi huushughulikia binadamu kwa mkono mkarimu, bila kusababisha matatizo yasiyoweza kutatulika, bila kuweka mtu yeyote katika shida; je, si hivi ndivyo? Ingawa watu idadi kubwa hawanipendi, bila kukasirishwa na mtazamo wa aina hii, Nimewapa wanadamu uhuru, kuwaruhusu hiari kiasi kwamba nimewaacha kuogelea pote katika bahari chungu. Kwa kuwa mtu ni chombo na hastahili kudhaminiwa: Ingawa yeye huona baraka Ninayoibeba mikononi Mwangu, hana shauku ya kuifurahia, ila angefurahia kuchomoa mjeledi kutoka kwa mkono wa Shetani matokeo yake yakiwa ni kujihukumu mwenyewe kumung’unywa na Shetani kama “chakula”. Bila shaka, kuna wengine ambao wameiona nuru Yangu kwa macho yao, na kwa hivyo, hata kama wao wanaishi katika ukungu wa wakati huu, hawajapoteza imani katika

mwanga kwa ajili ya ukungu huu wenye giza, lakini wameendelea kupapasa na kutafuta kupitia kwa ukungu—ijapokuwa katika njia ilichozagazwa vikwazo. Mwanadamu anaponiasi, Mimi humwelekezea hasira Zangu zenye ghadhabu, na kwa hivyo mwanadamu anaweza kuangamia kwa ajili ya kutotii kwake. Anaponitii, Mimi hubaki nimejificha kutoka kwake, kwa njia hii nikiamsha pendo katika kina cha moyo wake, pendo ambalo halinuii kunibembeleza, ila kunipa raha. Ni mara nyingi sana, katika uchunguzi wa mwanadamu kunipata, Nimefunga macho Yangu na kukaa kimya, kwa kusudi la kuvuta imani yake ya kweli. Lakini wakati Nimekosa kuongea, imani ya mwanadamu hubadilika ghafula, na hivyo kile Ninachokiona tu ni “mali” ghushi, kwa sababu mwanadamu hajawahi kunipenda kwa dhati. Ni wakati tu Ninapojidhihirisha Mwenyewe ndiyo kwamba binadamu wote hufanya onyesho kubwa la “imani”; lakini wakati Nimejificha katika pahali Pangu pa siri, wanakua dhaifu na kudhoofika moyo, kama kwamba wanahofia kunikosea; kuna hata baadhi ambao, kwa kuwa hawawezi kuuona uso Wangu, “wananipitisha katika mchakato mkubwa” hivyo kukanusha ukweli wa kuwepo Kwangu. Watu wengi hubaki katika hali hii; watu wengi wana fikira za aina hii. Ni upendeleo tu wa wanadamu wote kuficha yale mabaya ndani yao. Kwa sababu ya hili, hawako radhi kutangaza dosari zao wenyewe, na hukubaliana na ukweli wa maneno Yangu tu shingo upande na kwa nyuso zilizofichwa.

Machi 17, 1992

Sura ya 19

Ni wajibu wa mwanadamu kuchukua maneno Yangu kama msingi wa maisha yake. Mwanadamu lazima aanzishe fungu lake binafsi katika kila sehemu ya maneno Yangu; kutofanya hivyo kutakuwa kujiletea maangamizo na kujiletea dharau. Binadamu haunijui, na kwa sababu ya hili, badala ya kuleta maisha yake Kwangu badala, anachofanya ni kujipanga tu mbele Yangu na takataka mikononi mwake, na hivyo kujaribu kuniridhisha. Lakini, mbali na kuridhishwa na mambo yalivyo, Naendelea kutoa matakwa kwa binadamu. Napenda michango ya mwanadamu, lakini Nachukia madai yake. Wanadamu wote wana mioyo iliyojaa ulafi; ni kama moyo wa binadamu unadhibitiwa na Shetani, na mwanadamu hawezi kuponyoka na kutoa moyo wake Kwangu. Ninapozungumza, watu husikiliza sauti Yangu kwa makini sana; Ninaponyamaza kimya, hata hivyo, wao huanza “shughuli” zao wenyewe na kuacha kabisa kusikiliza maneno Yangu, kana kwamba maneno Yangu yalikuwa tu kijalizo cha “shughuli” zao. Sijawahi kuwa mzembe kwa binadamu, na bado Nimekuwa pia mwenye subira na mvumilivu kwa binadamu. Na hivyo, kwa sababu ya huruma Yangu, binadamu wote hujiinua na wanakosa maarifa na kujitafakari; wanatumia vibaya uvumilivu Wangu ili kunidanganya. Hakuna mmoja kati yao anayenijali kwa dhati, na hakuna mmoja kweli ananithamini kama kitu apendacho moyoni mwake; ni wakati tu walipo na wakati wa ziada ndipo wanaponitambua kwa kiwango

duni. Juhudi ambazo Nimetumia kwa mwanadamu tayari ni zaidi ya kipimo. Ninamfanyia mwanadamu aina ya pekee ya kazi, na mbali na haya, Nimempaa mzigo wa ziada, ili, ndani ya kile Ninacho na kile Nilicho, mwanadamu anaweza kupata maarifa na kupitia mabadiliko. Siwataki watu wawe ‘watumiaji’ tu; pia Nawataka wawe ‘wazalishaji’ wanaomshinda Shetani. Ingawa Sidai chochote kutoka kwa mwanadamu, hata hivyo Nina viwango vya matakwa Ninayoyatoa, kwani kuna madhumuni kwa yale Ninayoyafanya, na vile vile msingi wa matendo Yangu: Sichezi kiholela, anavyodhani mwanadamu, wala Siundi mbingu na dunia na mambo mengi ya uumbaji kwa ghafla na bila mpango. Kwa kazi Zangu, mwanadamu anapaswa kuwa na uwezo wa kuona kitu, kupata kitu. Hapaswi kutumia vibaya uchangamfu wa ujana wake, ama kutunza maisha yake kama vazi ambalo linakusanya vumbi; badala yake, anapaswa kujilinda vikali, kuchukua kutoka kwa fadhila Yangu kwa ajili ya starehe yake mwenyewe, hadi, kwa sababu Yangu, hawezi kumrudia Shetani, na kwa sababu Yangu anamshambulia Shetani. Si Ninachomwulizia mwanadamu ni rahisi hivi?

Mwangaza hafifu unapoanza kuonekana Mashariki, watu wote ulimwenguni wanautilia maani zaidi kidogo. Bila kujawa na usingizi, binadamu wanasonga mbele kuchunguza chanzo cha mwangaza huu wa mashariki. Kwa sababu ya uwezo wao finyu, hakuna yeyote ambaye ameweza kuona mahali unapotokea mwangaza. Wakati yote yaliyo ulimwenguni yameangaziwa kabisa, binadamu watazinduka kutoka usingizini na ndotoni, na ni hapo tu ndipo wanapotambua pole pole kwamba siku Yangu inawajia. Binadamu wote wanasherehekea kwa sababu ya ujio wa mwangaza, na kwa sababu ya haya hawalali tena, na si wapumbavu tena. Chini ya mng’aro wa mwangaza Wangu, binadamu wote wanakuwa na uwazi wa akili na mtazamo, na ghafla wanakuwa na furaha ya maisha. Chini ya kifuniko cha ukungu, Naulinda ulimwengu. Wanyama wote wako katika mapumziko; kwa sababu ya ujio wa mwangaza hafifu, kila kitu katika uumbaji kinafahamu kwamba maisha mapya yanakaribia. Kwa sababu hii, wanyama pia wanatoka nje ya mapango yao, kutafuta chakula. Mimea, bila shaka, si tofauti, na kwa mng’aro wa mwangaza majani yao ya kijani yanang’aa, yakisubiri kutakasa sehemu yao binafsi Kwangu wakati Niko duniani. Wanadamu wote wanataka ujio wa mwangaza, lakini bado wanahofia ujio wake, na wasiwasi kwamba ubaya wao hutafichika tena, kwani mwanadamu yu uchi kabisa, na hajafunikwa. Watu wangapi wanahofia, kwa sababu ya ujio wa mwangaza, na kwa sababu mwangaza umetokea, wako katika hali ya mshtuko? Watu wengi, baada ya kuuona mwangaza, hujawa na majuto yasiyo na mipaka, wakichukia uchafu wao, ilhali, bila uwezo wa kubadilisha ukweli, hawana budi ila kunisubiri Nitoe hukumu. Watu wangapi, wakisafishwa na mateso gizani, wanapooni mwangaza wanapigwa ghafla na umuhimu wake mkubwa, na hatimaye kukumbatia mwangaza karibu na vifua vyao, wakiogopa sana kuupoteza tena. Watu wengi sana, badala ya kutupwa nje ya uzingo na kutoka kwa ghafla kwa mwanga, wanaendelea tu na kazi ya

kila siku, kwa sababu wamekuwa vipofu kwa miaka mingi, na hivyo hawana habari kwamba mwangaza umekuja, wala hawaridhishwi nao. Katika mioyo ya binadamu, Mimi daima si wa juu, wala duni. Kulingana na wao, haijalishi kama Nipo au la; ni kama kwamba maisha ya mwanadamu hayawezi kuwa na upweke zaidi iwapo Sipo, na iwapo Nipo, hayatafaidika na furaha. Kwa sababu wanadamu hawanithamini, raha Ninayowapa ni chache. Lakini punde tu binadamu unaponiabudu kidogo, basi pia Nitafanya mabadiliko kwa mtazamo Wangu kwa binadamu. Kwa sababu hii, wakati tu binadamu unapofahamu sheria hii, ndipo tu wanadamu watakapokuwa na bahati ya kujitolea Kwangu na kudai vitu vilivyo mikononi Mwangu. Hakika pendo la mwanadamu Kwangu halifungwi tu na maslahi yake mwenyewe? Hakika imani yake Kwangu haifungwi tu kwa mambo Ninayompa? Inaweza kuwa kwamba, isipokuwa tu yeye kuona mwangaza Wangu, mwanadamu hawezi kunipenda kwa dhati kwa njia ya imani yake? Hakika nguvu za mwanadamu na afya hazizuiliwi na hali ya leo? Inaweza kuwa kwamba mwanadamu anahitaji ujasiri ili anipende?

Kutegemea kuwepo Kwangu, mambo mengi ya uumbaji yanakubali kwa utiifu mahali yanamoishi, na katu, bila ya nidhamu Yangu, hayajihusishi na uasherati bila kujali. Kwa hiyo, milima inakuwa mipaka kati ya mataifa ulimwenguni, maji yanakuwa vikwazo vya kuwatenga watu wa nchi tofauti mbali mbali, na hewa inapuliza kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine katika nafasi zilizo juu ya dunia. Binadamu tu ndio hawawezi kweli kutii matakwa ya mapenzi Yangu; hii ndiyo maana Nasema kwamba, kwa viumbe vyote, mwanadamu pekee ni ndiye wa kundi la wasiotii. Mwanadamu hajawahi kweli kunitii, na kwa sababu hii wakati wote Nimemweka chini ya nidhamu kali. Iwapo katikati ya binadamu, itakuja kuwa kwamba utukufu Wangu umetandaa ulimwengu nzima, basi hakika Nitachukua utukufu Wangu wote na kuufanya uwe wazi mbele ya mwanadamu. Kwa sababu katika uchafu wake mwanadamu hafai kutazama utukufu Wangu, kwa maelfu ya miaka Sijawahi kujitokeza hadharani, lakini Nimebakia mafichoni; kwa sababu hii utukufu Wangu hujawahi kuwa wazi mbele ya mwanadamu, na mwanadamu daima amezama kwa shimo la kina la dhambi. Nimeusamehe udhalimu wa binadamu, lakini wanadamu hawajui jinsi ya kujihifadhi, na badala yake daima wanajiweka wazi kwa dhambi, kuruhusu dhambi kuwajeruhi. Huu si ukosefu wa mwanadamu wa kujiheshimu na kujipenda? Katikati ya binadamu, kuna kweli yeyote anayeweza kupenda? Ibada ya mwanadamu inaweza kuwa na uzito wa wakia ngapi? Hakuna bidhaa safi zilizochanganywa na kinachoitwa uhalisi wake? Si ibada yake imeungana kabisa na mkanganyiko? Ninachohitaji ni upendo wa mwanadamu usiogawanyika. Mwanadamu hanijui, na ingawa anaweza kupata kunijua, hatanipa moyo wake wa ukweli na dhati. Kwa mwanadamu, Sidai kile asichotaka kupeana. Akinipa ibada yake, Nitaikubali bila pingamizi; lakini asiponiadini, na kukataa kujitoa hata kidogo Kwangu, badala ya kukasirika juu ya hayo, Nitamwondoa tu kwa njia ingine na kumpangia hatima

inayomfaa. Radi, inayovingirika angani, itawaangusha binadamu; milima ya juu, inapoanguka, itawazika; wanyama pori kwa njaa yao watawala; na bahari, zinapobingirika, zitawagubika. Binadamu wanapojishughulisha na migogoro ya mauaji ya jamii, binadamu wote watatafuta maangamizo yao katika majanga yatokayo katikati yao.

Ufalme unapanuka miongoni mwa binadamu, unachipua miongoni mwa binadamu, unasimama miongoni mwa binadamu; hakuna nguvu inayoweza kuharibu ufalme Wangu. Kwa watu Wangu walio katika ufalme wa leo, nani kati yenu si mwanadamu miongoni mwa wanadamu? Nani kati yenu yu nje ya hali ya ubinadamu? Wakati hatua Yangu ya kwanza mpya itatangazwa kwa wengi; binadamu utaguswa vipi? Mmeona na macho yenu hali ya mwanadamu; hakika bado hamna matumaini ya kudumu milele kwa dunia hii? Sasa Natembea ng'ambo katikati ya watu Wangu, Naishi katikati ya watu Wangu. Leo, walio na pendo la kweli Kwangu, watu kama hawa wamebarikiwa; wamebarikiwa wanaonitii, hakika watabaki katika ufalme Wangu; wamebarikiwa wanaonijua, hakika watakuwa na mamlaka katika ufalme Wangu; wamebarikiwa wanaonitafuta, hakika watatoroka vifungo vya Shetani na kufurahia baraka ndani Yangu; wamebarikiwa wanaoweza kujiacha, hakika wataingia katika milki Yangu, na kurithi fadhila ya ufalme Wangu. Wanaokimbia kimbiba kwa ajili Yangu Nitawakumbuka, wanaopata gharama kwa ajili Yangu Nitawakumbatia kwa furaha, wanaonitolea sadaka Nitawapa starehe. Wanaopata raha ndani ya maneno Yangu, Nitawabariki; hakika watakuwa nguzo zinazoshikilia mwamba kwa ufalme Wangu, hakika watakuwa na fadhila isiyo na kifani kwa nyumba Yangu, na hakuna anayeweza kulinganishwa nao. Mmewahi kuzikubali baraka mlizopewa? Mmewahi kuzitafuta ahadi mlizofanyiwa? Hakika, chini ya mwongozo wa mwangaza Wangu, mtapenya katika utawala wa nguvu za giza. Hakika, katikati ya giza, hamtaupoteza mwangaza unaowaongoza. Hakika mtakuwa bwana wa viumbe vyote. Hakika mtakuwa washindi mbele ya Shetani. Hakika, wakati wa maangamizi ya ufalme wa joka kubwa jekundu, mtasimama miongoni mwa umati mkubwa kushuhudia ushindi Wangu. Hakika mtasimama imara na thabiti katika nchi ya Sinimu. Kupitia katika mateso mnayoyavumilia, mtarithi baraka zinazotoka Kwangu, hakika mtaonyesha utukufu Wangu katika ulimwengu mzima.

Machi 19, 1992

Sura ya 20

Utajiri wa jumba Langu ni bila idadi na usioeleweka, lakini mwanadamu hajawahi kuja Kwangu kuufurahia. Hana uwezo wa kuufurahia mwenyewe, wala wa kujilinda mwenyewe kwa kutumia juhudi zake mwenyewe; badala yake, yeye daima huweka imani yake kwa wengine. Kati ya wale wote Ninaowatazamia, hakuna mtu aliyewahi kunitafuta kwa makusudi na moja

kwa moja. Wao wote huja mbele Zangu kwa kushawishiwa na wengine, wakiwafuata watu wengi, na hawana nia ya kulipa gharama au kutumia muda kustawisha maisha yao. Kwa hivyo, miongoni mwa watu hakuna mtu aliyewahi kuishi katika hali halisi, na watu wote huishi maisha yasiyo na maana. Kwa sababu ya njia na desturi za mwanadamu zilizoanzishwa kitambo, miili ya watu wote imejawa na harufu ya udongo wa ardhini. Kwa sababu hii, binadamu amekuwa asiyehisi, asiye na hisia zozote kwa ukiwa wa ulimwengu, na yeye badala yake hujishughulisha na kazi ya kujifurahisha ndani ya dunia hii iliyoganda. Maisha ya mwanadamu hayana joto hata kidogo, na hayana ubinadamu wala mwanga wowote—lakini daima amekuwa mwenye kujishughulisha na mwenyewe, akivumilia maisha yasiyo ya thamani ambayo yeye huenda hapa na pale akiharakisha kufanya mambo bila kufikia kitu chochote. Kwa haraka sana, siku ya kufa inakaribia, na mtu anakufa kifo cha uchungu. Katika dunia hii, yeye hajawahi fanikisha kitu chochote, au kufaidi na kitu chochote—yeye hufika tu kwa haraka, na kwa haraka anaondoka. Hakuna yeyote miongoni mwa wale walio machoni Mwangi amewahi kuleta chochote wala kuchukua chochote, kwa hivyo mwanadamu anahisi kwamba dunia haina haki. Lakini hakuna anayenuia kuondoka kwa haraka. Wanangoja kwa hamu siku ambayo ahadi Yangu kutoka mbinguni itatimizika ghafla miongoni mwa watu, ikiwaruhusu, wakati ambapo wamepotea, kwa mara nyingine tena kutazama njia ya uzima wa milele. Kwa hivyo, binadamu hutazama kwa makini kila tendo Langu na hatua ili kuona kama Mimi kweli nimetimiza ahadi Yangu kwake. Wakati yeye yuko katika mateso, au katika maumivu makali, au amekumbwa na majaribio na anakaribia kuanguka, binadamu hulaani siku ya kuzaliwa kwake akikusudia kuondokewa na taabu zake na aelekee mahali palipo pema. Lakini wakati majaribio yanapopita, binadamu hujawa na furaha. Anaadhimisha siku ya kuzaliwa kwake duniani na ananiomba Niibariki siku yake ya kuzaliwa; wakati huu, binadamu huwa hataji tena viapo vya zamani, anahofu sana kwamba kifo kitamjia mara ya pili. Mikono Yangu inapoinua dunia, watu hucheza kwa furaha, hawaoni tena huzuni, na wao wote wananitegemea Mimi. Ninapoufunika uso Wangu kwa mikono Yangu, na kuwasukuma watu chini ya ardhi, mara moja wao hupungukiwa na pumzi, na ni vigumu waweze kuishi. Wao wote hunililia, wakiwa wenye hofu kwamba Nitawaangamiza, kwa maana wote wanatamani kutazama siku ambayo Nitatukuzwa. Mwanadamu huchukua siku Yangu kama mtaji wa uwepo wake, na ni kwa sababu tu ya matarajio ya watu ya wakati utukufu Wangu utafika kwamba mwanadamu anaishi mpaka leo. Baraka iliyotoka kwa kinywa changu ni kwamba wale waliozaliwa katika siku za mwisho ni wenye bahati ya kutosha kuona utukufu Wangu wote.

Katika enzi zote, wengi wametoweka duniani kwa taabu, na kusita, na wengi wamekuja duniani kwa matumaini na imani. Nimeandaa kuja kwa wengi, na pia Nimewaondoa wengi. Watu wengi wamepitia mikono Yangu. Roho nyingi zimetupwa Kuzimu, wengi wameishi katika

mwili, na wengi wamekufa na wamezaliwa upya duniani. Hata hivyo kamwe hakuna yeyote kati yao aliyepata nafasi ya kufurahia baraka za ufalme leo. Mimi nimewapa wanadamu mengi sana, lakini wamepata kidogo, lakini kwa sababu mashambulizi ya jeshi la Shetani imewafanya wasiweze kufurahia utajiri Wangu wote. Amekuwa tu na bahati nzuri ya kuangalia juu, lakini hajawahi kuwa na uwezo wa kujifurahisha kikamilifu. Mwanadamu hajawahi gundua nyumba ya hazina mwilini mwake ili kupokea utajiri wa mbinguni, kwa hivyo amepoteza baraka ambazo Nimempa. Je, si roho ya mwanadamu ndio haswa uwezo wa kumuunganisha na Roho Wangu? Mbona mwanadamu hajawahi Kunihusisha na roho yake? Mbona ananikaribia kimwili na asiweze kunikaribia kiroho? Je, sura Yangu ya kweli ni ya kimwili? Mbona mwanadamu hatambui kiini Changu? Kuna uwezekano kuwa hakujawahi kuonekana ishara yoyote Yangu ndani ya roho ya mwanadamu? Je, Nimetoweka kabisa katika roho ya mwanadamu? Ikiwa mwanadamu hataingia katika ulimwengu wa kiroho, atawezaje kufahamu nia Zangu? Je, kuna chochote machoni mwa mwanadamu ambacho kinaweza penyeza moja kwa moja mpaka ulimwengu wa kiroho? Ni mara nyingi Nimemwita mwanadamu kwa Roho Wangu, lakini matendo yake huwa ni kama amechomwa kisu na Mimi, anahusiana nami kwa umbali, katika hofu kubwa kuwa Nitamwongoza kwenda ulimwengu mwingine. Kwa mara nyingi Nimepeleleza ndani ya moyo wa mwanadamu, lakini anabaki bila ufahamu kabisa, akiwa na hofu kubwa kabisa kuwa Nitaingia nyumbani mwake na kuchukua fursa hiyo kumnyang'anya mali yake yote. Kwa hivyo, ananifungia nje, kuniacha bila chochote ila mlango uliofungwa na kukazwa na kuniacha nje kwenye baridi. Ni mara nyingi mwanadamu ameanguka na Nimemwoko, lakini baada ya kuamka ananiacha mara moja, bila kuguswa na upendo Wangu, mwanadamu kunipiga macho ya hadhari; Sijawahi pasha joto moyo wa mwanadamu. Mwanadamu ni kiumbe kikatili kisichokuwa na hisia. Hata kama amepashwa joto na kumbatio Langu, kamwe hajawahi guswa na jambo hili. Mwanadamu ni kama kiumbe katili cha mlimani. Hajawahi thamini upendo Wangu wa binadamu. Hana nia ya kunikaribia, akipendelea kukaa katika milima, ambapo anavumilia tishio la wanyama pori—lakini bado hana nia ya kuchukua makao ndani Yangu. Simshawishi mwanadamu yeyote: Ninafanya tu kazi Yangu. Siku itawadia ambapo mwanadamu ataogelea kuja upande Wangu kutoka katikati ya bahari kuu, ili aweze kufurahia mali yote ya dunia na kuacha hatari ya kumezwa na bahari.

Kwa kuwa maneno Yangu yametimilika, ufalme utaumbwa duniani hatua kwa hatua na mwanadamu atarudishwa kwa ukawaida hatua kwa hatua, na hivyo basi kutaanzishwa duniani ufalme ndani ya moyo Wangu. Katika ufalme, watu wote wa Mungu hupata maisha ya mwanadamu wa kawaida. Msimu wa barafu yenye baridi kali umeenda, umebadilishwa na dunia ya miji ya majira ya chipuko, ambapo majira ya chipuko yanashuhudiwa mwaka mzima. Kamwe, watu hawakumbwi tena na ulimwengu wa mwanadamu wenye huzuni na wenye taabu,

na hawavumilii kuishi kwenye baridi kali ya dunia ya mwanadamu. Watu hawapigani na wenzao, mataifa hayaendi vitani dhidi ya wenzao, hakuna tena uharibifu na damu imwagikayo kutokana na uharibifu huo; maeneo yote yamejawa na furaha, na kila mahali pote panafurikwa na joto baina ya wanadamu. Naenda Nikipitia dunia nzima, Nafurahia kutoka juu ya kiti Changu cha enzi, Naishi miongoni mwa nyota. Na malaika wananipa nyimbo mpya na dansi mpya. Udhaifu wao hausababishi machozi kutiririka nyusoni mwao tena. Sisikii tena, mbele Yangu, sauti za malaika wakilia, na hakuna tena anayeninung'unikia kuwa ana shida. Leo hii, nyote mko hai mbele Yangu; kesho nyote mtakua hai ndani ya ufalme Wangu. Je, si hii ndiyo baraka kubwa zaidi ambayo Nimempa mwanadamu? Kwa sababu ya gharama ambayo mnalipa leo, mtarithi baraka za wakati ujao na mtaishi ndani ya utukufu Wangu. Je, si bado mnataka kujihusisha na kiini cha Roho Wangu? Je, bado mnataka kujiua wenyewe? Watu wako tayari kufuata ahadi ambazo wanaweza kuziona, hata kama ni za muda mfupi, lakini hakuna aliye tayari kukubali ahadi za kesho, hata kama ni za milele. Vitu vinavyoonekana kwa mwanadamu ni vitu ambavyo Nitaangamiza, na vitu visivyoweza kushikika na mwanadamu ndivyo Nitakavyotimiza. Hii ndiyo tofauti ya Mungu na mwanadamu.

Mwanadamu amehesabu siku Yangu, lakini hakuna yeyote amewahi jua siku kamili, na hivyo mtu anaweza kuishi tu katikati ya mzubao. Kwa sababu matamania ya mwanadamu huvuma katika anga isiyo na kikomo, halafu inapotea, mwanadamu amepoteza tumaini mara kwa mara tena, hadi ameshuka kwa hali yake ya sasa. Lengo la matamko Yangu si kumfanya mwanadamu kufuata tarehe, wala si kumsukuma aangamie kwa sababu ya kukata tamaa. Natamani kumfanya mwanadamu akubali ahadi Yangu, na Ninatamani watu duniani kote kuwa na mgawo wa ahadi Yangu. Kile Ninachotaka ni viumbe walio hai ambao wamejawa na uzima, si maiti ambazo zimegubika katika kifo. Kwa kuwa Ninaketi mezani pa ufalme, Nitatoa amri kwa watu wote duniani ili wapate ukaguzi Wangu. Siruhusu uwepo wa kitu chochote kisicho safi mbele Yangu. Sivumilii uwezekano wa mtu yeyote kuingilia kazi Yangu; wale wote ambao huingilia kati kazi Yangu wanatupwa katika gereza la chini ya ardhi, na baada ya kuachiliwa huru bado watakabiliwa na janga, watapokea miale ya moto ya kuunguza dunia. Wakati Mimi Niko katika hali yangu ya kimwili, yeyote anayepinga Kazi Yangu na mwili Wangu atanichukiza. Ni mara nyingi Nimewakumbusha wanadamu wote kwamba Mimi sina jamaa duniani, na yeyote aonaye kuwa Mimi ni sawa na yeye, na ananivuta kuja kwake ili aweze kupata kumbukumbu za nyakati za zamani na Mimi, ataangamia. Hii ndiyo amri Yangu. Katika masuala hayo Sina huruma kwa mwanadamu. Wale wote ambao huingilia kazi Yangu na hutoa ushauri Kwangu wanaadibiwa na Mimi, na kamwe Sitawasamehe. Kama Sizungumzi waziwazi, mwanadamu kamwe hataacha kufanya upumbavu kamwe, na ataanguka katika kuadibu Kwangu bila kujua—kwa kuwa mwanadamu hanijui katika nafsi ya mwili Wangu.

Sura ya 21

Mwanadamu huanguka katikati ya mwanga Wangu, na anasimama imara kwa sababu ya wokovu Wangu. Niletapo wokovu ulimwenguni kote, mwanadamu hujaribu kutafuta njia za kuingia miongoni mwa mtiririko wa urejesho Wangu, ilhali kuna watu wengi ambao huoshwa wasijulikane waliko na gharika hili la urejesho; kuna watu wengi ambao wamezama na kumezwa na mafuriko haya ya maji; na kuna watu wengi pia ambao husimama imara huku kukiwa na mafuriko, ambao hawajawahi kupoteza hisia zao za mwelekeo, na ambao basi wamefuata mafuriko mpaka sasa. Ninaenda hatua kwa hatua na mwanadamu, lakini yeye hajawahi kunitambua; yeye anajua tu nguo Ninazovaa kwa nje, na hajui utajiri uliofichika ndani Mwangu. Ingawa Mimi humruzuku mwanadamu na kumpa kila siku, hana uwezo wa kukubali kwa kweli, hana uwezo wa kupokea utajiri wote niliomba. Hakuna jambo lolote kuhusu upotovu wa mwanadamu ambalo huniepuka; Kwangu, ulimwengu wake wa ndani ni dhahiri kama mwezi unaong'aa juu ya maji. Mimi Simtendei mwanadamu katika njia iliyo hobelahobela wala kufanya mambo kwake kwa namna isiyo ya dhati; ni kwamba tu mwanadamu hawezi kujiwajibikia, na hivyo wanadamu wote daima wamepotoka, na hata wa leo bado hawana uwezo wa kujitoa wenyewe kutoka upotovu huo. Ole wao, maskini wanadamu! Kwa nini mwanadamu ananipenda lakini hawezi kufuata nia za Roho Wangu? Je, Mimi Sijajifichua kwa wanadamu kwa kweli? Wanadamu kwa kweli hawajapata kuuona uso Wangu kamwe? Je, inawezekana kwamba Nimeonyesha huruma kiasi kidogo sana kwa wanadamu? Enyi waasi wa wanadamu wote! Lazima waharibiwe chini ya miguu Yangu, ni lazima watokomee kabisa katikati ya kuadibu Kwangu, na lazima, siku ambayo mpango Wangu mkubwa utakamilika, watatupiliwa mbali kutoka kati ya wanadamu, ili wanadamu wote wazijue nyuso zao mbaya. Sababu ya mwanadamu kuona uso Wangu na kusikia sauti Yangu mara chache ni kwamba dunia nzima imejawa na machafuko sana, na kelele zake ni kubwa mno, na hivyo mwanadamu ni mvivu mno kutafuta uso Wangu na kujaribu kuelewa Moyo Wangu. Je, hii si sababu ya kupotoshwa kwa mwanadamu? Je, hii si ndiyo sababu mwanadamu yuko na mahitaji? Wanadamu wote daima wamekuwa katikati ya utoaji Wangu; kama isingekuwa hivyo, Nisingekuwa mwenye huruma, nani angenusurika mpaka leo? Utajiri Nilio nao hauna wa kulingana nao, na bado maafa yote yamo mikononi Mwangu—na ni nani awezaye kuepuka maafa wakati wowote apendapo? Je, maombi ya mwanadamu yanaweza kumruhusu afanye hivyo? Au machozi yaliyo moyoni mwa mwanadamu? Mwanadamu hajawahi kuniomba Mimi kwa kweli, na hivyo miongoni mwa wanadamu wote hakuna mwanadamu aliyewahi kuishi maisha yake yote kwenye mwanga wa ukweli, na watu wanaishi katikati ya mwanga unaooneka kwa kipindi pekee. Hii ndiyo

imesababisha mahitaji ya mwanadamu leo.

Kila mwanadamu ana hamu kubwa, tayari kufanya jambo lolote kwa sababu Yangu ili apate kitu kutoka Kwangu, na hivyo, nikizingatia saikolojia ya mwanadamu, Mimi humpa ahadi za kuhamasisha upendo wa kweli ndani yake. Je, ni upendo wa kweli wa mwanadamu unaompa nguvu? Je, ni uaminifu wa mwanadamu Kwangu ndio umegusa Roho Wangu mbinguni? Mbingu haijawahi kuathiriwa na matendo ya mwanadamu hata kidogo, na iwapo kumtendea Kwangu mwanadamu kungetegemea matendo yake yote, basi wanadamu wote wangeishi katikati ya kuadibu Kwangu. Nimewaona watu wengi wakitiririkwa na machozi, na Nimewaona watu wengi wakitoa nyoyo zao ili wapate utajiri Wangu. Licha ya “uchaji Mungu” kama huu, Sijawahi kujitoa kwa mwanadamu kikamilifu kwa sababu ya hisia zake za ghafla, kwa sababu mwanadamu hajawahi kuwa radhi kujitoa kwa furaha mbele Yangu. Nimeng’oa barakoa za watu wote na kutupa barakoa hizo katika ziwa la moto, na kama matokeo, unaodaiwa kuwa uaminifu wa mwanadamu na maombi yake hayajawahi kuwa imara mbele Zangu. Mwanadamu ni kama wingu angani: Wakati upepo unavuma, anahofia uwezo mkubwa wa nguvu yake na hivyo huelea kwa haraka kufuata upepo, akiwa na woga sana kuwa ataangamizwa kwa sababu ya uasi wake. Je, huu sio uso mbaya wa mwanadamu? Je, hili silo linalodaiwa kuwa utiifu wa mwanadamu? Je, hii siyo “hisia ya kweli” na nia njema bandia ya mwanadamu? Watu wengi hukataa kushawishiwa na maneno yote yatokayo kwenye kinywa Changu, na wengi hawakubali tathmini Yangu, na hivyo maneno na matendo yao hufichua nia zao za kuasi. Nisemacho ni kinyume cha asili ya zamani ya mwanadamu? Je, si Nimepeana ufafanuzi wa kufaa kwa binadamu kulingana na “sheria za asili”? Mwanadamu hanitii kwa kweli; angenitafuta kwa kweli, haingenibidi kusema mengi. Mwanadamu ni takataka isiyo na maana, na ni lazima Nitumie kuadibu Kwangu kumlazimisha kuendelea mbele; Nisingefanya hivyo,—ingawa ahadi Ninazompa ni za kutosha starehe yake—moyo wake ungeweza kushawishiwa vipi? Mwanadamu ameishi na mapambano machungu kwa miaka mingi; inaweza kusemekana, siku zote ameishi kwa kukata tamaa. Matokeo yake ni kuwa ameachwa kama amekufa moyo, na amechoka kimawazo na kimwili, na hivyo hapokei utajiri Ninaompa kwa furaha. Hata leo, hakuna mwanadamu aliye na uwezo wa kukubali utamu wote wa roho kutoka Kwangu. Watu wanaweza tu kubaki maskini, na kusubiri siku ya mwisho.

Watu wengi wangependa kunipenda kwa kweli, lakini kwa sababu mioyo yao si yao wenyewe, hawawezi kujidhibiti wenyewe; watu wengi hunipenda kwa kweli katika majaribio Ninayotoa, lakini hawana uwezo wa kuelewa kwamba Mimi kwa kweli Nipo, na wanapenda tu katikati ya utupu; na si kwa sababu ya kuwepo Kwangu halisi; watu wengi, baada ya kuweka nyoyo zao mbele Zangu, hawazijali, na hivyo nyoyo zao zinanyakuliwa na Shetani wakati wowote anapopata nafasi, na baada yake huniacha; watu wengi hunipenda kwa dhati Ninapotoa

maneno Yangu, lakini hawathamini maneno Yangu katika roho zao, badala yake wakiyatumia kwa kawaida kama mali ya umma na kuyatupa yalipotoka wakati wowote wanapotaka. Mwanadamu hunitafuta akiwa na maumivu, na hunitazamia akiwa na majaribu. Wakati kuna amani yeye hunifurahia, wakati wa hatari yeye hunikana, wakati ana kazi nyingi yeye hunisahau, na asipokuwa na kitu cha kufanya yeye hufanya vitu kwa namna isiyo ya dhati—lakini kamwe hakuna yeyote ambaye amenipenda katika maisha yake yote. Ningependa mwanadamu awe mwenye bidii mbele Zangu: Mimi Simuombi chochote, ila tu watu wote wanichukulie kwa umakini, kwamba, badala ya kunirairai, waniruhusu kurudisha uaminifu wa mwanadamu. Nuru Yangu, mwangaza na gharama ya juhudi Zangu huenea kwa watu wote, ilhali hivyo pia ukweli halisi wa kila tendo la mwanadamu huenea kwa watu wote, kama ufanyavyo wao kunidanganya. Ni kama kwamba viungo vya udanganyifu wa mwanadamu vimekuwa naye tangu tumboni mwa mamake, kama kwamba amekuwa na mbinu hizi maalum za kuhadaa tangu kuzaliwa kwake. Kuzidisha, hajawahi kufichua siri yake; hakuna mwanadamu aliyewahi kutambua chanzo cha ujuzi huu wa udanganyifu. Matokeo yake ni kuwa mwanadamu anaishi katika udanganyifu bila kujua, na ni kana kwamba yeye hujisamehe mwenyewe, kana kwamba ni mipango ya Mungu na sio yeye kunidanganya. Je, hiki sicho chanzo halisi cha mwanadamu kunidanganya? Je, huu sio mpango wake wa ujanja? Sijawahi kuchanganywa na ushawishi na hila za mwanadamu, kwa maana Mimi Nilishatambua kiini chake muda mrefu uliopita. Nani anayejua kiasi cha uchafu ulio katika damu yake, na kiasi gani cha sumu ya Shetani kimo ndani ya mafupa yake? Mwanadamu anapata uzoefu wa sumu hii kila uchao, hata anakosa busara ya kufahamu maafa ya Shetani na hivyo hana nia ya kutambua “sanaa ya uwepo wa afya.”

Wakati mwanadamu yuko mbali nami, na wakati ananijaribu, Mimi hujificha kutoka kwake kati ya mawingu. Na hivyo, hawezi kunipata hata kidogo, na huishi tu mikononi mwa waovu, akifanya yote watakayo. Mwanadamu anaponikaribia, Mimi hujitokeza kwake na sifichi uso Wangu kutoka kwake, na kwa wakati huu, mwanadamu huona hisia ya ukarimu usoni Mwangu. Yeye ghafla hupata fahamu na ingawa hatambui, ndani yake kunazaliwa upendo Kwangu. Katika moyo wake, yeye ghafla huhisi utamu usio na kifani, na hustaajabu jinsi gani hakuweza kutambua kuwepo Kwangu ulimwenguni. Hivyo basi mwanadamu ana hisia kubwa ya uzuri Wangu, na zaidi, ya thamani Yangu kubwa. Matokeo, yake ni kuwa yeye hatamani kamwe kuniacha tena, Ananiona kama mwanga wa maisha yake, na akiwa na woga sana kuwa Naweza kumwacha, hunikumbatia kwa nguvu. Mimi siguswi na bidii ya mwanadamu, lakini ni mwenye rehema kwake kwa sababu ya upendo wake. Kwa wakati huu, mwanadamu mara moja huishi katikati ya majaribio Yangu. Uso Wangu hutoweka kutoka moyo wake, na yeye mara moja huona kuwa maisha yake ni matupu na anafikiria kukimbia. Wakati huu, moyo wa mwanadamu huwekwa wazi. Yeye hanikumbatii kwa sababu ya tabia Yangu, lakini ananiomba Nimlinde kwa

sababu ya upendo Wangu. Hata hivyo, upendo Wangu unapomgeukia mwanadamu, yeye mara moja hubadili mawazo yake; yeye hukiuka agano lake nami na hujiweka mbali na hukumu Yangu, asiwe na nia ya kutazamia uso Wangu wa rehema tena, na hivyo hubadilisha mtazamo wake Kwangu na husema kuwa Sijawahi kumwokoia mwanadamu. Je, upendo wa kweli unahusisha huruma pekee? Je, mwanadamu ananipenda tu akiishi chini ya mwanga Wangu unaong'aa? Yeye anaangalia ya jana lakini anaishi katika wakati huu—si hizi ni hali za mwanadamu? Je, kesho mtakuwa jinsi mliyoy bado? Ninachotaka ni mwanadamu awe na moyo unaonitamani kwa kina na sio moyo unaoniridhisha na vitu vya juu juu.

Machi 21, 1992

Sura ya 22

Mwanadamu anaishi katikati ya mwanga, ilhali hana habari kuhusu thamani ya mwanga huo. Hana ufahamu kuhusu kiini cha mwanga huo, na chanzo cha mwanga huo, na, zaidi ya hayo, hajui mmiliki wake ni nani. Ninapotuza mwanga huo miongoni mwa binadamu, papo hapo Ninachunguza hali ilivyo miongoni mwa wanadamu: Kwa sababu ya mwanga huo, watu wote wanabadilika, na wanakua, na wametoka gizani. Ninaangalia kila pembe ya ulimwengu, na Ninaona kuwa milima yote imefunikwa na ukungu, kwamba maji yameganda kwa ajili ya baridi, na kwamba, kwa sababu ya kuja kwa mwanga, watu wanatazama Mashariki ili wapate kuona kitu kilicho na thamani zaidi—ilhali mwanadamu bado hana uwezo wa kutambua njia ya wazi kwenye ukungu huo. Kwa sababu dunia nzima imefunikwa kwa ukungu, Ninapotazama kutoka mawinguni, kuwepo Kwangu hakujawahi kutambuliwa na mwanadamu; mwanadamu anatafuta kitu fulani duniani, anaonekana akichakura, anayo nia, inaonekana, ya kusubiri kurudi Kwangu—ilhali yeye hajui siku Yangu, na anaweza tu kutegemea mara kwa mara mwanga unaong'aa mashariki. Miongoni mwa watu wote, Ninatafuta wale wanaoupendeza moyo Wangu kwa kweli. Natembea miongoni mwa watu wote, na kuishi miongoni mwa watu wote, lakini mwanadamu yuko salama salimini duniani, na kwa hivyo hakuna wanaoupendeza nafsi Yangu kwa kweli. Watu hawajui jinsi ya kuyajali mapenzi Yangu, hawawezi kuona matendo Yangu, na hawawezi kutembea katika mwanga na kumulikwa na mwanga huo. Hata ingawa mwanadamu daima anayathamini maneno Yangu, yeye hana uwezo wa kuona katika mikakati ya udanganyifu ya Shetani; kwa kuwa kimo cha mwanadamu ni kidogo sana, hana uwezo wa kufanya vile ambavyo moyo wake unatamani. Mwanadamu hajawahi kunipenda kwa dhiti. Ninapompandisha, yeye hujiona asiyefaa, lakini hili halimfanyi awe na ari ya kuniridhisha. Yeye hushikilia tu nafasi Niliyompa mikononi mwake na kukichunguza; bila hisia yoyote kwa uzuri Wangu, yeye anasisitiza badala yake kujijaza na baraka za kituo chake. Je, huu sio upungufu wa mwanadamu? Milima inaposonga, je, inaweza kubadili mkondo kwa ajili ya kituo chako? Maji

yanaposonga, je, yanaweza kukoma kabla ya kufikia kituo cha mwanadamu? Je, mbingu na dunia zinaweza kubadilishwa na kituo cha mwanadamu? Wakati mmoja Nilikuwa mwenye huruma kwa mwanadamu, mara kwa mara—ilhali hakuna anayependa kwa dhati wala kuthamini haya, waliyasikiliza tu kama hadithi, au waliisoma tu kama tamthilia. Je, maneno Yangu hayauguza moyo wa mwanadamu? Je, matamshi Yangu kwa kweli hayaleti mabadiliko yoyote? Inawezekana kuwa hakuna anayeamini katika kuwepo Kwangu? Mwanadamu hajipendi mwenyewe; badala yake, anaungana na Shetani ili kunivamia Mimi, na kumtumia Shetani kama “chombo” cha kunitumikia Mimi. Nitapenyeza katika mipango yote ya Shetani, na kuwazuia watu wote wa duniani dhidi ya kukubali uongo wa Shetani, ili wasije wakaniasi Mimi kwa ajili ya kuwepo kwa Shetani.

Katika ufalme, Mimi ni Mfalme—lakini badala ya kunichukulia kama Mfalme, mwanadamu ananichukulia kama Mwokozi aliyeshuka kutoka mbinguni. Kwa sababu hii, anasubiri kwa hamu Nimpe sadaka, na hafuatili ufahamu Wangu. Wengi sana wamelia mbele Zangu kama waombaji; wengi pia wamenifungulia “mifuko” yao na kunisihi Niwape chakula ili waendeleo kuishi; wengi wao wameniwekea macho yenye tamaa, kama mbwa mwitu wenye njaa, wakitamani wanibugie na kujaza matumbo yao; wengi pia wameinamisha vichwa vyao kwa sababu ya dhambi zao na kuona aibu, wakiomba huruma Yangu, au kukubali adhabu Yangu kwa hiari. Ninapozungumza, makosa kadhaa ya mwanadamu yanaonekana ya upuuzi, na umbo lake la kweli linaonekana katika mwanga, na katika mwangaza unaong’aa, mwanadamu hana uwezo wa kujisamehe mwenyewe. Hivyo, anakimbia na kuinama mbele Zangu na kutubu dhambi zake. Kwa sababu ya “uaminifu” wa mwanadamu, Mimi Namvuta tena kwa mara nyingine kwenye gari la wokovu, na kwa sababu hii mwanadamu ana shukurani Kwangu, na kunitupia jicho la upendo. Ilhali bado hana nia ya kujificha kikamilifu ndani Yangu, na hajautoa moyo wake wote Kwangu. Yeye anajigamba tu kwa ajili Yangu, ilhali hanipendi kwa kweli, kwa maana hajaweka mawazo yake Kwangu; mwili wake uko mbele Yangu, ilhali moyo wake uko nyuma Yangu. Kwa sababu kuelewa kwa mwanadamu kwa sheria ni kwa chini sana na hana haja ya kuja mbele Yangu, Mimi Nampa usaidizi unaofaa, ili aweze kugeuka upande Wangu kutoka kati ya upumbavu wake uliokita mizizi. Hii hasa ndiyo huruma ninayompa mwanadamu, na ndiyo njia ambayo nafanya bidii ili kumwokoia mwanadamu.

Watu ulimwenguni kote wanasherehekea kufika kwa siku Yangu, na malaika wanatembea miongoni mwa watu Wangu wote. Shetani anapoleta vurugu, malaika, kwa sababu ya huduma yao mbinguni, daima huwasaidia watu Wangu. Wao hawadanganywi na ibilisi kwa sababu ya udhaifu wa binadamu, ila wanapata uzoefu mwingi wa maisha ya mwanadamu yaliyojawa na ukungu unaosababishwa na uvamizi wa nguvu za giza. Watu wote wananyenyekea chini ya jina Langu, na hakuna wakati ambapo mtu huiuka kwa wazi kunipinga Mimi. Kwa sababu ya

shughuli za malaika, mwanadamu anakubali jina Langu na wote wako katika mtiririko wa kazi Yangu. Dunia inaanguka! Babeli imelemaa! Dunia ya kidini—itakosa kuharibiwa vipi na mamlaka Yangu duniani? Ni nani bado anathubutu kuniasi na kunipinga? Waandishi? Wakuu wote wa kidini? Viongozi na wenye mamlaka wa duniani? Malaika? Ni nani asiyesherehekea ukamilifu na wingi wa mwili Wangu? Miongoni mwa watu wote, nani asiyeimba sifa Zangu bila kukoma, ni nani asiye na furaha isiyoshindwa? Ninaishi katika nchi ya kiota cha joka kubwa jekundu, ilhali hili halinifanyi Mimi nitetemeke kwa uoga wala kutoroka, kwa maana watu wa nchi hii wote wameanza kulichukia. Hakuna wakatia ambapo kitu chochote kimefanya “wajibu” wake mbele ya joka kwa sababu ya joka hili; badala yake, vitu vyote vinatenda kama vinavyoona kuwa bora, na kila kitu kinaenda kufanya shughuli zake. Je, mataifa ya ulimwengu yatakosaje kuangamia? Mataifa ya ulimwengu yatakosaje kuanguka? Watu Wangu watakosaje kushangilia? Watakosaje kuimba kwa furaha? Je, hii ni kazi ya mwanadamu? Je, ni tendo la mikono ya mwanadamu? Nilimpa mwanadamu mzizi wa kuwepo kwake, na Nikampa vitu halisi vya dunia, ilhali mwanadamu haridhiki na hali yake ya sasa na anauliza kuingia katika ufalme Wangu. Lakini atawezaje kuingia katika ufalme Wangu kwa urahisi vile, bila kulipa gharama yoyote, na bila nia ya kujitoa kwa kujinyima? Badala ya kulazimisha chochote kutoka kwa mwanadamu, Mimi huweka mahitaji kwake, ili ufalme Wangu duniani ujawe na utukufu. Mwanadamu ameongozwa na Mimi mpaka enzi ya sasa, anaishi katika hali hii, na anaishi katika mwongozo wa mwanga Wangu. Kama haingekuwa hivyo, nani kati ya watu wote duniani angejua matarajio yake? Ni nani ambaye angeelewa mapenzi Yangu? Ninaongeza matoleo Yangu katika mahitaji ya mwanadamu; je, hii haiambatani na sheria za hali asili?

Jana uliishi kati ya upepo na mvua, leo hii umeingia katika ufalme Wangu na kuwa watu wake, na kesho utafurahia baraka Zangu. Ni nani aliwahi kuwaza juu ya mambo kama haya? Je, ni dhiki na ugumu kiasi gani utakayopitia maishani mwako, je mnajua? Mimi naendelea kati ya upepo na mvua, na nimeishi mwaka baada ya mwingine miongoni mwa wanadamu, na hiyo inafuatwa na wakati wa sasa. Je, hizi sio hatua za mpango Wangu wa usimamizi? Ni nani amewahi kuongeza chochote katika mpango Wangu? Ni nani anaweza kuepuka hatua katika mpango Wangu? Naishi katika nyoyo za mamia ya mamilioni ya watu, Mimi ni Mfalme miongoni mwa mamia ya mamilioni ya watu, na nimekataliwa na kushutumiwa na mamia ya mamilioni ya watu. Mfano Wangu hauko kwa kweli ndani ya moyo wa mwanadamu. Mwanadamu anaona tu kwa umbali sura Yangu ya utukufu katika maneno Yangu, lakini kwa sababu ya hitilafu iliyo katika mawazo yake, haamini hisia zake mwenyewe; kuna uwepo Wangu usioeleweka vizuri ndani ya moyo wake, lakini uwepo huo haukai ndani yake kwa muda mrefu. Na kwa hivyo, upendo wake Kwangu pia uko vilevile: Upendo wake Kwangu unaonekana vizuri, ni kama kila mwanadamu alinipenda kutokana na tabia yake, kana kwamba upendo wake

ulikonyeza ndani na nje ya kuonekana chini ya mbalamwezi hafifu. Leo, ni kwa sababu tu ya upendo Wangu ndiyo maana mwanadamu bado yupo na ana bahati nzuri ya kunusurika. Kama haingekuwa hivyo, nani kati ya wanadamu, kwa sababu ya kunyauka kwa miili yao, asingeuawa na mwale wa moto? Mwanadamu bado hajielewi. Anajionyesha akiwa mbele Yangu, na kujigamba mwenyewe akiwa nyuma Yangu, ilhali hakuna anayethubutu “kuniasi” akiwa mbele Yangu. Hata hivyo, mwanadamu hajui maana ya upinzani Ninaozungumzia; badala yake, yeye anajaribu kunipumbaza Mimi, na anaendelea kujipandisha—na kwa hili, je, si ananipinga kwa wazi? Ninavumilia udhaifu wa mwanadamu, lakini Sina huruma hata kidogo kwa uasi ambao mwanadamu ameufanya mwenyewe kwa kujua. Hata ingawa anajua maana yake, yeye hana nia ya kutenda kulingana na maana hiyo na hutenda kutokana na kupenda kwake ananidanganya Mimi. Mimi huweka wazi mwenendo Wangu katika maneno Yangu kila wakati, ilhali mwanadamu hapataniki na kushindwa—na wakati uo huo, anadhihirisha mwenendo wake. Katika hukumu Yangu mwanadamu atashawishika kikamilifu, na katikati ya adhabu Yangu mwishowe ataweza kuishi kwa kudhihirisha mfano Wangu na kuwa udhihirisho Wangu duniani!

Machi 22, 1992

Sura ya 23

Ninapopaza sauti Yangu, macho Yangu yanapofyatua moto, Ninaitazama kwa uangalifu dunia nzima, Ninatazama kwa uangalifu ulimwengu mzima. Wanadamu wote wananiomba Mimi, wameinua macho yao kuelekea Kwangu, wakiomba Nipunguze hasira, na kuapa kutoniasi tena. Lakini haya siyo yaliyopita; bali yaliyopo kwa sasa. Ni nani anayeweza kubadilisha mapenzi Yangu? Kwa kweli sio sala katika moyo wa mwanadamu, wala maneno yanayotoka midomoni mwao? Ni nani ambaye ameweza kuishi hadi wakati huu, isipokuwa ni kwa nguvu Zangu? Ni nani anayeishi ila kwa maneno ya kinywa Changu? Ni nani asiyekaa chini ya uangalifu wa macho Yangu? Ninapofanya kazi Zangu katika ulimwengu mzima, ni nani ambaye ameweza kuiepuka kazi hiyo? Inawezekana kuwa milima imeiepuka kutokana na urefu wayo? Inawezekana kuwa maji kwa wingi na upana wake, yameweza kuizuia kazi hii? Katika mpango Wangu, Sijawahi kuachilia kitu chochote kiende kwa wepesi, hivyo basi hakuna mtu yeyote, wala kitu chochote, ambacho kimeepuka mikono Yangu. Hivi leo, jina Langu takatifu linatukuka katika uumbaji wote, na tena, maneno ya malalamiko katika binadamu dhidi Yangu yanachipuka, na hadithi kuhusu kuwepo Kwangu ulimwenguni zimeenea miongoni mwa binadamu. Sivumilii binadamu wanapotoa hukumu dhidi yangu, wala Sivumilii wao kuugawanya mwili Wangu, wala lugha ya machungu na matusi dhidi Yangu. Ukweli ni kuwa mwanadamu hajawahi kunifahamu Mimi, tangu awali amenikana na kuzua upinzani Kwangu, akishindwa kumpenda Roho Wangu au kuyathamini maneno ya kinywa Changu. Kwa kila tendo

na hatua yake, na kwa mtazamo wake Kwangu, Nampa binadamu “tuzo” yake inayomfaa. Hivyo basi, binadamu hufanya jambo wakiwa wameweka macho kwenye tuzo yao, na wala hapana mmoja aliyefanya kazi inayohusisha kujinyima na kujitolea. Wanadamu hawana nia ya kujitoa kwa kujinyima, ila wanafurahia tuzo zinazopatikana kwa kutofanya chochote. Japo kuwa Petro alijiweka wakfu mbele Zangu, haikuwa ni kwa sababu ya malipo ya kesho, bali kwa maarifa ya leo. Binadamu hawajawahi kushirikiana kwa kweli na Mimi, lakini muda baada ya muda ameweza kukumbana Nami kwa namna ya juujuu, hivyo kufikiria bila juhudi za kupata idhini Yangu. Nimeangalia kwa kina ndani ya moyo wa mwanadamu, na kuibua undani wake wa siri “mgodi wa utajiri mwingi,” kitu ambacho hata mwanadamu mwenyewe hafahamu lakini mimi Nimefahamu upya. Hivyo basi, mpaka watakapojionea kwa macho “ushahidi wa kuonekana”, hapo tu ndipo binadamu atasitisha unafiki wa kujidhalilisha mwenyewe na, mikono iliyonyooshwa watakubali hali yao ya uchafu. Miongoni mwa binadamu, kuna mambo mengi mapya na ya kisasa yanayoningoja Mimi “niwatolee” ili kila mwanadamu astarehe. Mbali na kutia kikomo katika kazi Yangu kwa ajili ya ukosefu wa uwezo kwa mwanadamu, Ninampogoa kama ilivyokuwa mpango Wangu wa awali. Binadamu ni kama mti wa matunda: bila ya kuukata na kuupogoa, mti huo hautaweza kuzaa matunda na, mwishowe, yatakayoonekana ni matawi yaliyonyauka na majani yaliyoanguka, pasipo na matunda yoyote kuanguka ardhini.

Ninapokipamba “chumba cha ndani” cha ufalme Wangu siku baada ya siku, hakuna yule ameingia katika “chumba Changu cha kazi” kwa ghafla ili kuvuruga kazi Yangu. Watu wote wanafanya wawezayo kushirikiana nami, wakiwa na hofu mno ya “kufukuzwa” na “kupoteza nafasi zao” hivyo kufikia tamati maishani mwao ambapo wanaweza kuanguka “jangwani” anakoishi Shetani. Kwa sababu ya uoga wa mwanadamu, Ninamfariji kila siku, Nikimwegemeza katika pendo kila siku na zaidi ya yote kumwelekeza na sheria kila siku ya maisha yake. Ni kana kwamba wanadamu wote ni watoto wachanga ambao wamezaliwa sasa hivi; bila ya kupewa maziwa, watatoweka duniani humu, wasipate kuonekana tena. Kati ya maombi ya unyenyekevu ya mwanadamu, Nakuja katika ulimwengu wa mwanadamu, na moja kwa moja, mwanadamu anaishi katika ulimwengu wenye mwanga, wasifungiwe tena katika “chumba” ambako wanatoa vilio vya maombi vikielekea mbinguni. Mara tu wanaponiona, binadamu kwa kusesitiza huleta mbele Yangu “maombolezo” yaliyo mioyoni mwao, wakifungua vinywa vyao mbele Yangu wakiomba kwamba chakula kiangukshwe midomoni mwao. Lakini baadaye, hofu yao kutoweka na hali tulivu kurejea, na hakuna wanachohitaji kutoka Kwangu tena, mwanadamu hulala fofofu au hukana uwepo Wangu, kisha kuelekea kufanya mambo yao wenyewe. Katika ile hali ya mwanadamu “kutelekeza”, ni wazi kuwa binadamu pasi na “hisia” huendeleza “haki bila mapendeleo” Kwangu. Hivyo basi, Ninapomwangalia mwanadamu katika ile hali yake ya ukosefu wa pendo Kwangu, Mimi huondoka kwa upole pasi na kurudi tena kwa wepesi katika

hali yake ya maombi ya hitaji. Bila ya mwanadamu kufahamu, shida zake zinaongezeka siku baada ya siku, hivyo, katika hali yake ya kufanya kazi kwa bidii, ndipo anapofahamu uwepo Wangu, yeye, akikataa kuchukua “la” kama jawabu, kisha anashika kwa nguvu nguo Yangu na kunikaribisha kwa ukarimu nyumbani kwake kama mgeni. Lakini, ingawa anaandaa chakula kitamu mbele Yangu ili Niweze kustarehe, hajawahi kunikubali kama mmoja wa wenzi wake, badala yake akinichukulia kama mgeni ili tu apate kitu kiasi kidogo cha usaidizi kutoka Kwangu. Hivyo basi mwanadamu kwa wakati huu anaweka wazi Kwangu hali yake ya kuhurumisha, akiwa na matumaini kuwa atapata “sahihi,” na, kama yule anayehitaji mkopo kwa ajili ya biashara yake, ananikabili kwa nguvu zake zote. Katika kila ishara yake na mwenendo, Ninapata mtazamo wa nia ya mwanadamu: ni kana kwamba, katika maoni yake, Mimi sijui kusoma maana fiche iliyo juu ya uso wa mwanadamu na kufichwa nyuma ya maneno atamkayo, au jinsi ya kuangalia ndani ya moyo wa mwanadamu. Hivyo basi binadamu huweka wazi uaminifu wake Kwangu kwa kila hali tuliyoandamana, bila ya kuwacha au kusahau jambo lolote, kisha kuyaleta madai yake kwangu. Nina machukizo dhidi ya kila tendo la mwanadamu. Miongoni mwa binadamu, hakuna yeyote yule aliyefanya tendo lililonipendeza, kana kwamba wanafanya makusudi ili kuniudhi, wakiwa na kusudi la kuvutia adhabu Yangu kali: Wote wakitia gwaride kushoto na kulia mbele Yangu, wakitenda yaliyo mapenzi yao mbele ya macho yangu. Hakuna yeyote kati ya binadamu anayeishi kwa ajili Yangu, hivyo basi kuwepo kwa viumbe vyote kunakosa maana na wanadamu wanaishi kwa utupu mkuu. Hata hivyo, binadamu bado wanakataa kutoka katika hali ile ya uzinifu wakiendelea na uasi wao Kwangu wakisisitiza kukaa katika ubatili.

Katika majaribu yote wanayopitia, wanadamu hawajawahi hata siku moja kunipendeza. Kwa sababu ya ukatili wa uovu wao, mwanadamu hana jitihada yoyote ya kueneza jina Langu; ila, “anakimbia upande mwingine” akinitegemea kumpa riziki ya kila siku. Mwanadamu hanipi moyo wake wote hivyo kumuelekeza shetani kumnyanyasa hadi akapata majeraha mengi, na mwili wake kujawa na uchafu. Lakini mwanadamu bado hafahamu jinsi uso wake ulivyo mbaya: muda huu wote akimwabudu Shetani kinyume na mapenzi Yangu. Kwa sababu hii, kwa hasira Nitamtupa mwanadamu katika shimo lisilo na mwisho, asiloweza kujitoa ndani. Hata hivyo, kati ya kulia kwake kwa kuhuzunisha, binadamu bado hukataa kubadilisha mawazo yake, akidhamiria kupingana Nami hadi mwisho wa machungu yake, akiwa na kusudi la kuzidisha ghadhabu Yangu. Kwa ajili ya yale aliyoyatenda, Ninamtendea kama mwenye dhambi na kumnyima joto la kumbatio Langu. Tokea mwanzo, malaika wamenihudumia na kuniheshimu bila ya kubadili mienendo, lakini mwanadamu kila mara akifanya kinyume, kana kwamba hakutoka Kwangu, ila kazaliwa na Shetani. Malaika katika maeneo yao hunipa ibada kamili; hawatikiswi na nguvu za kishetani, na wanatimiza tu wajibu wao. Wakiwa wamelishwa na

malaika, halaiki za Wanangu na watu Wangu wote hukua kwa nguvu na wenye afya, hakuna kati yao yeyote yule aliyedhoofika kiafya. Hii ni kazi ya mikono Yangu, muujiza Wangu. Kama vile vigelegele baada ya vigelegele vya moto wa kanuni huzindua uanzilishi wa ufalme Wangu, malaika, wakiwa wanatembea katika usawa wa kifuasi, huja mbele ya jukwaa Langu kujiwasilisha kwa ukaguzi, Wangu, kwa sababu mioyo yao haina uchafu na haiabudu miungu mingine, hivyo hawaepuki ukaguzi Wangu.

Upepo mkali unapovuma kwa mayowe, mbingu hushuka ghafla, na kufanya wanadamu kukosa hewa hivyo basi hawawezi tena kuliita jina Langu jinsi wapendavyo. Bila ya kujua, ubinadamu wote umeanguka. Miti huyumba mbele na nyuma katika upepo, mara kwa mara matawi husikika yakitoa sauti ya kuvunjika, na majani yote yaliyonyauka hubebwa na upepo. Dunia hujaa kiza na ukiwa mara moja, na watu wakikumbatiana kwa pamoja, wakingoja maafa yanayofuata majira ya kupukutika kwa majani kuwapata wakati wowote. Ndege milimani wakipuruka huku na kule, kana kwamba wanalia huzuni wao kwa mtu fulani; na katika pango za milima, simba hunguruma, wakiogofya watu kwa sauti zao, kufanya damu yao igande na kuogofya, ni kama kwamba kuna hisia ya kuogofya inayoashiria mwisho wa wanadamu. Bila kungojea furaha ya nia Yangu ya kuwaangamiza, binadamu wote huomba kimoyomoyo kwa Bwana Mkuu aliye mbinguni. Lakini itawezekanaje upepo mkubwa kuzuiliwa na kelele za maji yakitiririka kwenye kijito? Itawezekanaje upepo huu usimamishwe kwa sauti za sala za binadamu? Itawezekanaje hasira moyoni mwa radi kutulizwa sababu ya woga wa mwanadamu? Mwanadamu huyumba mbele na nyuma katika upepo; hukimbia huku na kule ili kujifichia mvua; na chini ya ghadhabu Yangu, binadamu hutingizika na kutetemeka, wakihofu kuwa Nitaweka mikono Yangu juu ya miili yao, kana kwamba Mimi ni ncha ya bunduki iliyoelekezwa katika kifua cha mwanadamu, na pia, ni kama yeye ni adui Yangu, ijapokuwa ni rafiki Yangu. Mwanadamu hajawahi kwa kweli kufahamu nia Yangu kwake, hajawahi hata siku moja kufahamu makusudi Yangu ya kweli hivyo basi bila ya kujua, hukosea dhidi Yangu, bila ya kujua, hunipinga, ilhali, bila kutaka, ameona kiasi cha upendo Wangu. Ni vigumu binadamu kuona uso Wangu wakati wa ghadhabu Yangu. Nimejificha nyuma ya mawingu ya hasira Yangu na Ninasimama, kati ya mingurumo ya radi, juu ya ulimwengu wote na kutuma huruma Zangu chini kwa mwanadamu. Kwa sababu ya mwanadamu kukosa maarifa kunihusu, Simwadibu kwa kukosa kujua nia Yangu kwake. Mbele ya macho ya binadamu, Mimi huweka wazi ghadhabu Yangu mara kwa mara, Ninatabasamu mara kwa mara, lakini hata anaponiona, mwanadamu kweli hajawahi kuona ukamilifu wa tabia Yangu, na bado hana uwezo wa kusikia kelele za furaha na uwazi, kwa sababu amejaa upumbavu na ujinga. Ni kana kwamba umbo Langu linakaa katika kumbukumbu ya mwanadamu, na nafsi Yangu katika mawazo yake. Hata hivyo, hapana Yule ambaye amewahi kuniona kwa kweli kati ya ukuaji wa wanadamu wote, kwa sababu akili

za binadamu zina upungufu wa hali ya juu. Kwa yote ambayo mwanadamu “amenichambua”, sayansi ya jamii ya mwanadamu haina mizizi na, kufikia sasa, utafiti wake wa kisayansi haujaibua matokeo kamilifu. Na hivyo basi, mada ya “umbo Langu” imekuwa daima tupu pasiwe na yeyote wa kuijaza, hakuna wa kuivunja rekodi ya dunia kwa sababu ili mwanadamu aweze kuweka mguu wake imara katika ulimwengu wa sasa ni kifuta machozi kisichokadirika katika matukio makuu yenye majonzi.

Machi 23, 1992

Sura ya 24

Kuadibu kwangu kunawajia watu wote, lakini pia kunakaa mbali na watu wote. Maisha yote ya kila mtu yamejaa upendo na pia chuki Kwangu, na hakuna mtu ambaye amewahi kunijua na kwa hivyo mtazamo wa mwanadamu Kwangu ni wa sitasita, na hauna uwezo wa kuwa kawaida. Lakini Nimekuwa Nikimlea na kumchungu mwanadamu na ni kwa sababu ya upumbavu wake ndiyo maana hana uwezo wa kuona matendo Yangu yote na kuelewa nia Zangu. Mimi Ndiye Ninayeongoza katika mataifa yote, na ndiye Mkubwa Zaidi kwa watu wote; kwa ufupi ni kwamba mwanadamu hanijui Mimi. Kwa miaka mingi Nimeishi na mwanadamu na kujionea Maisha katika dunia ya mwanadamu, lakini amekuwa Akinipuuzwa na kunichukulia kama kiumbe kutoka ulimwengu wa nje ya dunia. Kwa sababu hii, kutokana na tofauti za tabia na lugha, watu Huchukulia Mimi kama mgeni barabarani. Nguo Zangu, huenda ikawa, pia ni za kipekee, hata kumfanya mwanadamu kukosa imani ya kunikaribia. Ni wakati huo ndio naona upweke wa maisha ya mwanadamu, na wakati huo tu ndio Ninapata ufafanuzi wa dhuluma katika dunia ya mwanadamu. Ninatembea katikati ya wapita njia, Nikiangalia nyuso zao zote. Ni kama kwamba wanaishi ndani ya maradhi, ambayo yanajaza nyuso zao na huzuni, na miongoni mwa adhabu, inayozuia kuachiliwa kwao. Mwanadamu hujitia pingu mwenyewe na kuonyesha adabu. Watu wengi hujenga hisia za uwongo juu yao mbele Yangu ili Niwaunge mkono, na watu wengi hujifanya makusudi kuwa wa kuhuzunisha mbele Yangu ili waweze kupata usaidizi Wangu. Nyuma Yangu, watu wote wanairairai na kuniasi. Je, Mimi sio wa kweli? Je, huu si mkakati wa mwanadamu ili aweze kuishi? Ni nani ambaye ameweza kuishi kwa kunidhihirisha katika Maisha yake? Nani ambaye ameweza kunitukuza miongoni mwa wengine? Nani amewahi kuwajibika mbele ya Roho? Nani ambaye amesimama imara kwa ushuhuda wake Kwangu mbele ya Shetani? Ni nani ameweza kuongezea ukweli kwa hulka ya “uaminifu” walio nao Kwangu? Ni nani amewahi kutupwa nje na joka kubwa jekundu kwa sababu Yangu? Watu wametupa kura zao kwa shetani na sasa wanatembea naye kwenye matope, wamekuwa wataalam kwa Kunipinga, na wamekuwa waanzilishi wa upinzani kuja Kwangu, na ni “wanafunzi waliobobea” katika njia zao zisizo za dhati katika kunishughulikia. Kwa ajili ya hatima yake mwenyewe,

mwanadamu anatafuta hapa na pale duniani, na Ninapomwita, anabaki kutokuwa na uwezo wa kuhisi thamani Yangu kubwa na anaendelea kuwa na Imani katika kujitegemea, asiwe mzigo kwa wengine. “Matarajio” ya mwanadamu ni ya thamani, lakini hakujawahi kuwa na matarajio ya yeyote ambayo yametimiza alama zote. Yote yanabomoka mbele Yangu, na kuporomoka bila sauti.

Kila siku Ninaongea, na kila siku Nafanya mambo mapya pia. Ikiwa mwanadamu hawezi kutumia nguvu zake zote, basi atakuwa na ugumu kusikia sauti Yangu na atapata ugumu kuona uso wangu. Mpendwa Anaweza kuwa mzuri sana, na mazungumzo Yake kuwa yenye upole mkubwa sana, lakini mwanadamu hana uwezo wa kutazama kwa urahisi sura Yake tukufu na kusikia sauti Yake. Katika miaka yote, hakuna ambaye amewahi kuweza kutazama sura Yangu kwa urahisi. Niliwahi kuongea na Petro na Nikajitokeza kwa Paulo, na hakuna mwingine— isipokuwa Waisraeli—ambaye kweli amewahi kuona uso Wangu. Leo, nimekuja Mimi Mwenyewe kati ya mwanadamu kuishi pamoja na yeye. Je, hiki hakihisi kuwa kitu nadra na cha thamani kwenu? Je, hamtamani kufanya matumizi bora ya muda wenu? Je, mnataka jambo hili liwapite kwa njia hii? Inawezekana muda usimamishwe ghafula katika mawazo ya watu? Au inawezekana muda urudishwe nyuma? Au inawezekana mwanadamu awe kijana tena? Inawezekana maisha ya leo yenye baraka kuja tena? Simpatii mwanadamu “zawadi” sahihi kwa “ubadhirifu” wake. Mimi huendelea kufanya kazi Yangu tu, nimejitenga na mengine yote na sisimamishi mtiririko wa masaa kwa sababu mwanadamu ana shughuli, au kwa sababu ya sauti ya vilio vyake. Kwa miaka elfu kadhaa, hakuna ambaye ameweza kugawa nguvu Yangu, na hakuna ambaye ameweza kuharibu mpango Wangu wa asili. Nitavuka anga, na kuzunguka miaka, na kuanzisha kiini cha Mpango Wangu mzima juu na miongoni mwa vitu vyote. Hakuna mtu hata mmoja ambaye ameweza kupokea utunzaji maalum kutoka Kwangu au zawadi kutoka mikononi Mwangu, licha ya kwamba wanafungua vinywa vyao na kuomba ili wapate hivi vitu, licha ya kuwa wananyoosha mikono yao, huku wakisahau kila kitu kingine, wanataka hivi vitu kutoka Kwangu. Hakuna hata mmoja wa hawa watu amenisababisha kubadilisha nia Yangu, na wao wote wamesukumwa nyuma na sauti Yangu “isiyo na utu.” Watu wengi bado wanaamini kuwa wao ni “wachanga sana,” na hivyo wanasubiri Niwaonyeshe rehema kubwa, kuwa na huruma kwao kwa mara ya pili, na wanauliza Niwaruhusu kuchukua mlango wa nyuma. Hata hivyo ni jinsi gani Mimi Nitaufanyia mpango Wangu mzaha? Je, Ninaweza kusimasisha dunia isizunguke kwa ajili ya ujana wa mwanadamu, ili aweze kuishi miaka zaidi duniani? Akili ya mwanadamu ni tata, lakini inaonekana kwamba pia kuna vitu ambavyo inakosa. Kwa sababu hii, katika akili ya mwanadamu mara nyingi huonekana “njia za ajabu” za kupinga kazi Yangu kwa makusudi.

Ingawa ni mara nyingi Nimesamehe dhambi za mwanadamu, na kumwonyesha upendeleo

wa pekee kwa sababu ya udhaifu wake, mara nyingi pia Nimempa utunzaji sahihi kwa sababu ya ujinga wake. Ni rahisi kuwa mwanadamu hajawahi kujua jinsi ya kufahamu wema Wangu, hadi amezama ndani ya yale anayopitia sasa: amefunikwa katika vumbi, nguo zake zikiwa matambara, nywele zake zimefunika kichwa chake kama magugu yanayokua, uso wake umepakwa masizi, miguu yake imevalishwa viatu valivyojitengenezea yaye mwenyewe, mikono yake kama makucha ya tai aliyekufa, yakining'inia kwa udhaifu katika pande zake. Nikifungua macho Yangu na kutazama, ni kama kwamba mwanadamu amepanda juu kutoka nje ya shimo lisilo na mwisho. Sina budi ila kuwa na hasira: Nimekuwa mvumilivu kwa mwanadamu, ni jinsi gani Nilimruhusu shetani kuja na kwenda kama atakavyo kutoka Ufalme Wangu mtakatifu? Ni jinsi gani nilimruhusu mwombaji kula bure katika nyumba Yangu? Ni jinsi gani nilivumilia kuwa na roho mchafu kama mgeni wa nyumba Yangu? Mwanadamu daima amekuwa “mkali kwake mwenyewe” na “mwenye upole kwa wengine,” ilhali hajawahi angalau hata kidogo kuwa na adabu kuelekea Kwangu, maana Mimi ni Mungu mbinguni, na hivyo Yeye hunichukulia Mimi kwa nia tofauti, na hajawahi kuwa na upendo hata kidogo Kwangu. Ni kama kwamba macho ya mwanadamu ni majanja: Mara tu anapokutana na Mimi, uso wake unabadilika mara moja na anaongeza hisia kidogo kwa uso wake baridi na usio na hisia. Mimi simtilii mwanadamu vikwazo vinavyofaa kwa sababu ya mtazamo wake kuelekea Kwangu, bali Naangalia tu angani kutoka juu ya ulimwengu na kutekeleza kazi Yangu hapa duniani. Katika kumbukumbu ya mwanadamu, sijawahi kuonyesha wema kwa mtu yeyote, lakini sijawahi pia kumtendea vibaya mtu yeyote. Kwa sababu mwanadamu hanihifadhii “kiti kitupu” ndani ya moyo wake, Nisipotahadhari na kukaa ndani yake, ananilazimisha Mimi Nitoke nje bila utaratibu, na kisha anatomia maneno ya kujipendekeza na ubembelezaji ili kufanya visingizio, akisema yeye hana uwezo wa kujitoa mwenyewe kwa ajili ya starehe Yangu. Anapoonzea, uso wake mara nyingi hufunikwa na “mawingu ya giza,” kana kwamba madhara yatakuja miongoni mwa wanadamu wakati wowote. Hata hivyo, bado ananiambia Mimi niondoke, bila kuzingatia hatari zinazohusika. Hata kama ninampatia mwanadamu maneno Yangu na joto la kumbatio Langu, yeye anaonekana kuwa hasikii, na hivyo haipatii sauti Yangu muda hata kidogo, na badala yake anashikilia kichwa chake huku akiondoka upesi. Naondoka kwa mwanadamu Nikijihisi Nimesikitishwa kidogo, lakini pia nikiwa Nimeghadhabishwa. Mwanadamu wakati huo anatoweka huku kukiwa na shambulio la upepo mkubwa na mawimbi makuu. Baadaye, Ananililia Mimi, lakini ni jinsi gani yeye angebadili harakati ya upepo na mawimbi? Hatua kwa hatua, dalili zote za mwanadamu zinapotea, mpaka hapatikani mahala popote.

Kabla ya nyakati, Niliangalia nchi zote za ulimwengu kutoka juu mbinguni. Nilipanga shughuli kubwa duniani: uumbaji wa mwanadamu ambaye angependeza moyo Wangu, na ujenzi wa ufalme duniani kama ule wa mbinguni, Nikaruhusu uwezo Wangu kujaza anga na hekima

Yangu kuenea kote ulimwenguni. Na hivyo leo, maelfu ya miaka baadaye, Mimi Naendelea na mpango Wangu, lakini hakuna anayejua mpango Wangu au usimamizi wa dunia, wala hawauoni ufalme Wangu duniani. Kwa hivyo, mwanadamu hukimbiza vivuli, na kuja mbele Yangu ili kujaribu kunidanganya, akitaka kulipa “gharama ya kimya” ili apate baraka Zangu za mbinguni. Kwa sababu hii, amechochea hasira Yangu na Ninamletea hukumu, lakini bado hana fahamu. Ni kana kwamba alikuwa anafanya kazi kichinichini, pasi na kutojua kabisa lililokuwa likiendelea katika ulimwengu huku akifuata ndoto na dhamira zake tu. Miongoni mwa watu wote, sijawahi kuona mtu yeyote ambaye anaishi chini ya mwanga Wangu. Wanaishi katika ulimwengu wa giza, na wanaonekana kuzoea kuishi ndani ya giza. Mwanga unapokuja wanakaa mbali, na ni kana kwamba mwanga umevuruga kazi zao; matokeo yake, wanaonekana kuudhika kidogo, ni kama mwanga umeathiri amani yao na kuwaacha bila uwezo wa kulala fofofu. Kwa sababu hii, mwanadamu anakusanya nguvu zake zote na kuuondoa mwanga. Mwanga, pia, unaonekana kukosa ufahamu, na hivyo unaamsha mwanadamu kutoka usingizini, na wakati mwanadamu anaamka, anafunga macho yake, akijawa na hasira. Kwa kiasi fulani ni kama hajafurahishwa na Mimi, lakini katika moyo Wangu najua lengo. Ninaendelea hatua kwa hatua kuimarisha mwanga, kusababisha watu wote kuishi katika mwanga Wangu, ili baada ya muda usiokuwa mrefu wazoe kujihusisha na mwanga, na, zaidi ya hapo, wote wathamini mwanga huo. Kwa wakati huu, ufalme Wangu umekuja miongoni mwa mwanadamu, watu wote wanacheza kwa shangwe na kusherehekea, ghafla dunia inajazwa na furaha, na kimya cha miaka elfu kadhaa chavunjwa kwa kuwasili kwa mwanga ...

Machi 26, 1992

Sura ya 25

Muda unapita, na kufumba na kufumbua leo imefika. Chini ya uongozi wa Roho Wangu, watu wote wanaishi katikati ya mwanga Wangu, na hakuna anayefikiria yaliyopita ama kuiwekea jana maanani. Nani hajawahi kuishi katika wakati wa sasa? Ni nani ambaye hajapitia katika siku na miezi ya ajabu katika ufalme? Ni nani hajaishi chini ya jua? Ingawa ufalme umeshuka miongoni mwa mwanadamu, hakuna ambaye amepata kupitia ukunjufu wake; mwanadamu anautambua tu kutoka nje, bila kufahamu dutu lake. Wakati ambapo ufalme Wangu unatengenezwa, ni nani asiyefurahi kwa sababu yake? Je, nchi katika dunia zinaweza kuutoroka kweli? Je, joka kubwa jekundu linaweza kutoroka kwa msaada wa ujanja wake? Amri Zangu za utawala zinatangazwa katika ulimwengu wote, zinaasisi mamlaka Yangu miongoni mwa watu wote, na zinatumika katika ulimwengu wote; hata hivyo, mwanadamu hajawahi kweli kuyafahamu haya. Wakati amri Zangu za utawala zinafichuliwa kwa ulimwengu ndipo pia wakati kazi Yangu duniani itakuwa karibu kukamilika. Nitakapotawala na kuonyesha nguvu

miongoni mwa wanadamu wote na Nitakapotambulika kuwa Mungu mmoja Mwenyewe, ufalme Wangu utashuka duniani kikamilifu. Leo, watu wote wana mwanzo mpya kwenye njia mpya. Wameanza maisha mapya, ilhali hakuna yule ambaye amewahi kwa kweli kuyapitia maisha duniani sawa na mbinguni. Je, mnaishi kweli katika mwanga Wangu? Je, mnaishi kweli miongoni mwa maneno Yangu? Ni nani asiyetilia maanani matarajio yake mwenyewe? Ni nani asiye na wasiwasi kuhusu hatima yake? Nani hapambani katika bahari ya mateso? Ni nani asiyetaka kujiweka huru? Je, baraka za ufalme ni kwa sababu ya bidii ya mwanadamu duniani? Je, tamaa zote za mwanadamu zinaweza kutimizwa jinsi anavyotaka? Siku moja Nilionyesha mandhari mazuri wa ufalme mbele wa mwanadamu, ilhali aliuangalia tu kwa macho ya ulafi na hakuna aliyetamani kuingia. Wakati mmoja “Niliripoti” hali ya kweli ya dunia kwa mwanadamu, ila hakufanya chochote zaidi ya kusikiza, na hakutazama maneno yaliyotoka katika mdomo Wangu na moyo wake; siku moja Nilimwambia mwanadamu kuhusu hali ya mbinguni, ilhali aliyachukua maneno Yangu kama hadithi za maajabu, na hakukubali kweli kile ambacho mdomo Wangu ulieleza. Leo, matukio ya ufalme yanaangaza miongoni mwa mwanadamu, lakini kuna mtu ambaye amewahi “kuvuka kilele na bonde” akiutafuta? Bila wito Wangu, mwanadamu asingekuwa ameamka kutoka kwenye ndoto zake. Je, ametekwa sana na maisha yake duniani kwa kweli? Kweli hakuna kiwango cha juu katika moyo wake?

Wale ambao Nimewaamulia kabla kama watu Wangu wanaweza kujitoa Kwangu na kuishi kwa maelewano Nami. Ni wa thamani machoni Pangu, na wanang’aa na upendo Kwangu katika ufalme Wangu. Kati ya watu wa leo, ni nani anayetimiza masharti hayo? Nani awezaye kufikia kiwango kulingana na mahitaji Yangu? Mahitaji Yangu kweli yanaleta ugumu kwa mwanadamu? Je, Ninamfanya atende makosa kwa makusudi? Mimi mwenye huruma kwa watu wote, na Mimi huwachukulia kwa hali ya mapendeleo. Hata hivyo, hii tu ni kwa watu Wangu wa Uchina. Si kuwa Nawachukulia kwa hali ya chini ama kuwa Nawaangalia kwa wasiwasi, bali ni kwamba Mimi Nawachukua kwa matendo na hali halisi. Watu hukutana na vikwazo katika maisha yao bila kuepuka, kama ni kuhusu familia zao ama dunia kwa upana. Ilhali ugumu wa nani umepangwa kwa mikono yao wenyewe? Mwanadamu hana uwezo wa kunijua. Ana ufahamu wa mwonekano Wangu wa nje, ilhali hajui dutu Yangu; hajui viungo vya vyakula akulavyo. Ni nani anaweza kuona kwa uangalifu moyo Wangu? Nani anaweza kuelewa kweli mapenzi Yangu mbele Yangu? Nikija chini duniani, giza limetanda na mwanadamu “amelala fofofu.” Natembea miongoni mwa mahali pote, na yote Nionayo ni yaliyoraruka na matambara na yasiyoweza kuvumilia kuyaona. Ni kana kwamba mwanadamu yuko radhi tu kufurahia, na hana tamaa yoyote kufuata “vitu vya nje, ya ulimwengu.” Bila kujulikana kwa watu wote, Ninaaua ulimwengu mzima, ilhali sioni mahala popote ambapo pamejaa uzima. Hapo papo, Ninaangaza mwanga na joto na kutazama dunia kutoka mbingu ya tatu. Ingawa mwangaza

unaanguka juu ya ardhi na joto inatawanyika juu yake, mwangaza na joto pekee ndizo zinaonekana kufurahi; haziamshi chochote kutoka kwa mwanadamu, ambaye anafurahia kwa raha. Ninapoona haya, Ninarejesha mara moja kwa mwanadamu “fimbo” ambayo Nimetayarisha. Fimbo inapoanguka, mwangaza na joto vinatawanywa hatua kwa hatua na dunia mara moja inakuwa ya kuhuzunisha na yenye giza—na kwa sababu ya giza, mwanadamu anatawaa nafasi kuendelea na raha. Mwanadamu ana busara ndogo kuhusu kuwadia kwa fimbo Yangu, lakini haonyeshi hisia, na anaendelea kufurahia baraka zake duniani. Inayofuata, mdomo Wangu unatangaza adhabu kwa wanadamu wote, na watu katika ulimwengu wote watasulubiwa msalabani vichwa vikiangalia chini. Adhabu Yangu inapokuja, mwanadamu anatingizwa na kelele ya milima ikitikisika na ardhi ikipasuka, na baadaye anashtuliwa. Akiwa ameshtuka na mwoga, anatamani kutoroka, lakini ameshachelewa. Adhabu Yangu inapoanguka, ufalme Wangu unashuka juu ya dunia na nchi zote zinapasuliwa kuwa vipande, vipipotea bila kueleza na kutoacha chochote nyuma.

Kila siku Natazama juu ya uso wa ulimwengu, na kila siku Nafanya kazi Yangu mpya kati ya mwanadamu. Ilhali watu wote wanazama kwa shughuli za kazi,” na hakuna anayetilia maanani mienendo ya kazi Yangu ama kugundua hali ya vitu zaidi ya wao wenyewe. Ni kana kwamba watu wanaishi katika mbingu mpya na dunia mpya waliotengeneza wenyewe, na hawataki mtu mwingine kuingilia kati. Wote wameshiriki katika kazi ya kujifurahisha, wanajitamani wakifanya “mazoezi ya kimwili.” Kweli hakuna mahali Pangu katika moyo wa mwanadamu? Mimi hakika sina uwezo wa kuwa mtawala wa moyo wa mwanadamu? Roho ya mwanadamu kweli imemwacha? Nani amewahi kuyatafakari kwa makini maneno kutoka kwa mdomo Wangu? Nani amewahi kutambua ombi la moyo Wangu? Je, moyo wa mwanadamu kweli umechukuliwa na kitu kingine? Wakati mwingi sana Nimepaza sauti Nikimwita mwanadamu, lakini je, kuna yule ambaye amehisi huruma? Je, kuna yeyote ambaye amewahi kuishi katika ubinadamu? Mwanadamu anaweza kuishi katika mwili, lakini hana ubinadamu. Je, alizaliwa katika ufalme wa wanyama? Ama alizaliwa mbinguni, na anamilikiwa na uungu? Ninafanya madai Yangu kwa mwanadamu, ilhali ni kana kwamba haelewi maneno Yangu, kana kwamba Mimi ni jitu la kutisha, lililo geni kwake. Mara nyingi Nimevunjwa matumaini na mwanadamu, mara nyingi Nimekasirishwa na utendaji kazi wake duni, na ni mara nyingi Nimesikitishwa na unyonge wake. Mbona sina uwezo wa kuibua hisia ya kiroho katika moyo wa mwanadamu? Mbona Sina uwezo wa kuvuta upendo katika moyo wa mwanadamu? Mbona mwanadamu hataki kunichukulia kama kipenzi chake? Je, moyo wa mwanadamu sio wake mwenyewe? Je, kitu kingine kimechukua makao katika roho yake? Mbona mwanadamu anaomboleza bila kukoma? Ni kwa nini yeye ana taabu? Mbona, wakati yuko na huzuni, hajali uwepo Wangu? Je, inaweza kuwa kwamba Mimi nimemdunga mwanadamu? Je, inawezekana

kwamba Nimemwacha mwanadamu kwa makusudi?

Machoni Pangu, mwanadamu ndiye mtawala wa vitu vyote. Nimempa mamlaka si haba, Nikimwezesha kusimamia vitu vyote duniani—nyasi iliyo juu ya milima, wanyama katika misitu, na samaki majini. Badala ya kuwa na furaha kwa sababu ya haya, mwanadamu anasumbuliwa na wasiwasi. Maisha yake yote ni yale ya maumivu makali, na kukimbia hapa na pale, na raha kuongezwa kwa utupu, na katika maisha yake yote hakuna uvumbuzi na uundaji mpya. Hakuna anayeweza kujinasua kutoka katika utupu huu wa maisha, hakuna ambaye amegundua maisha ya maana, na hakuna ambaye amepitia maisha ya kweli. Ingawa watu wa leo wote wanaishi chini ya mwanga Wangu unaong’aa, hawajui lolote kuhusu maisha ya mbinguni. Nisipokuwa na huruma kwa mwanadamu na Nisipomwokoa binadamu, basi watu wote wamekuja bure, maisha yao duniani hayana maana, na wataondoka bure, bila chochote cha kujigamba nacho. Watu wa kila dini, nyanja ya jamii, taifa, na dhehebu wote wanajua utupu ulio duniani, na wote wananitafuta na kungoja kurejea Kwangu—ilhali nani ana uwezo wa kunifahamu nitakapofika? Nilitengeneza vitu vyote, niliumba binadamu, na leo nimeshuka kati ya mwanadamu. Mwanadamu, lakini, anagonga nyuma Yangu, na kulipisha kisasi Kwangu. Je, kazi Ninayofanya kwa mwanadamu haina faida yoyote kwake? Je, Mimi hakika sina uwezo wa kumtosheleza mwanadamu? Mbona mwanadamu ananikataa? Mbona mwanadamu ni baridi na hana hisia Kwangu? Mbona ardhi imejawa na maiti? Je, hii ndiyo hali ya dunia Niliyomtengenezea mwanadamu? Mbona Nimempa mwanadamu mali isiyo ya kufananishwa, ilhali ananipa Mimi mikono miwili mitupu? Mbona mwanadamu hanipendi kwa kweli? Mbona haji kamwe mbele Zangu? Maneno Yangu yote yamekuwa ya bure? Je, maneno yamepotea jinsi joto lipoteavyo kwa maji? Mbona mwanadamu hataki kushirikiana na Mimi? Je, wakati wa kufika kwa siku Yangu ni wakati wa kufa kwa mwanadamu kweli? Je, hakika Ningeweza kumwangamiza mwanadamu wakati ufalme Wangu utatengenezwa? Mbona, wakati wa mpango Wangu wa usimamizi wote, hakuna ambaye ameweza kuelewa nia Zangu? Mbona, badala ya kuyatunza matamshi ya kutoka kwa mdomo Wangu, mwanadamu anayachukia na kuyakataa? Simkashifu yeyote, ila tu Nawafanya watu wote watulie na kutekeleza kazi ya kujiangalia kwa undani.

Machi 27, 1992

Furahini, Enyi Watu Wote!

Katika nuru Yangu, watu wanaiona nuru tena. Katika neno Langu, watu wanapata mambo ambayo wanafurahia. Nimekuja kutoka Mashariki, Ninatoka Mashariki. Utukufu Wangu unapoangaza, mataifa yote yanatiwa nuru, vitu vyote vinaletwa kwenye mwanga, hakuna kitu

hata kimoja kinachobaki gizani. Katika ufalme, maisha ambayo watu wa Mungu wanaishi pamoja na Mungu ni yenye furaha kupita kiasi. Maji yanacheza kwa furaha katika maisha ya watu yenye baraka, milima inafurahia pamoja na watu katika wingi Wangu. Wanadamu wote wanajitahidi, wakifanya bidii, wakionyesha uaminifu wao katika ufalme Wangu. Katika ufalme, uasi haupo tena, upinzani haupo tena; mbingu na dunia zinategemeana, Mimi na mwanadamu tunakaribiana katika hisia ya kina, katika furaha kuu tamu ya maisha, tukiegemeana.... Wakati huu, Ninayaanza rasmi maisha Yangu mbinguni. Usumbufu wa Shetani haupo tena, na watu wanaingia katika pumziko. Ulimwenguni kote, watu Wangu wateule wanaishi ndani ya utukufu Wangu, wakiwa wamebarikiwa sana, si kama watu wanaoishi kati ya watu, lakini kama watu wanaoishi na Mungu. Binadamu wote wamepitia upotovu wa Shetani, na kuishi maisha ya mateso makubwa. Sasa, mtu anawezaje kutofurahia akiishi katika nuru Yangu? Mtu anawezaje kuuachilia wakati huu mzuri umponyoke? Enyi watu! Imbeni wimbo ulio mioyoni mwenu na mnichezee kwa furaha! Iinueni na mnitolee mioyo yenu ya dhati! Pigeni ngoma zenu na mnichezee kwa furaha! Ninaangaza furaha Yangu ulimwenguni kote! Naufichua uso Wangu mtukufu kwa watu! Nitaita kwa sauti kubwa! Nitaupita ulimwengu wote! Tayari Ninatawala kati ya watu! Ninatukuzwa na watu! Ninapeperuka kwenye mbingu zenye rangi ya samawati na watu wanakwenda wakitembea pamoja nami. Ninatembea kati ya watu na watu Wangu wananzunguka! Mioyo ya watu ni yenye furaha, nyimbo zao zinautikisa ulimwengu, zikiipasua mbingu! Ulimwengu haujafunikwa kwa ukungu tena; hakuna matope tena, hakuna mkusanyiko wa maji machafu tena. Watu watakatifu wa ulimwengu! Mnaonyesha nyuso zenu za kweli chini ya ukaguzi Wangu. Ninyi sio watu mliofunikwa na uchafu, lakini ni watakatifu walio safi kama jiwe la thamani lenye rangi ya kijani kibichi, ninyi nyote ni wapendwa Wangu, ninyi nyote ni furaha Yangu! Vitu vyote vinafufuka! Watakatifu wote wamerejea ili kunitumikia mbinguni, wakiingia katika kumbatio Langu lililo changamfu, hawalii tena, hawana wasiwasi tena, wakijitoa Kwangu, wakirudi nyumbani Kwangu, nao watanipenda bila kukoma katika nchi yao! Wasibadilike kamwe milele! Huzuni iko wapi! Machozi yako wapi! Mwili uko wapi! Dunia inapita, lakini mbingu ni za milele. Ninawaonekana watu wote, na watu wote wananisifu. Maisha haya, uzuri huu, tangu zama za kale hadi mwisho wa dahari, havitabadilika. Haya ndiyo maisha ya ufalme.

Sura ya 26

Ni nani ameshinda nyumbani Kwangu? Ni nani amesimama kwa ajili Yangu? Ni nani ameteseka kwa ajili Yangu? Ni nani ameweka ahadi yake mbele Zangu? Ni nani amenifuata hadi leo lakini hajakuwa wa kutojali? Mbona wanadamu wote wana ubaridi na hawana hisia? Mbona binadamu ameniacha? Mbona mwanadamu amechoka na Mimi? Mbona hakuna joto katika ulimwengu wa mwanadamu? Nikiwa Zayuni, Nimeonja joto lililo mbinguni, na Nikiwa Zayuni

Nimefurahia baraka iliyoko mbinguni. Tena, Nimeishi miongoni mwa binadamu, Nimeuhisi uchungu ulioko katika ulimwengu wa binadamu, Nimeona kwa macho Yangu hali zote tofauti zilizopo miongoni mwa wanadamu. Bila kujua, mwanadamu amebadilika pamoja na mabadiliko Yangu, na ni katika njia hii pekee ndio amepata kufika siku ya leo. Sihitaji kwamba mwanadamu aweze kufanya chochote kwa ajili Yangu, wala Sihitaji kwamba aongeze chochote kwa mujibu Wangu. Nataka tu aweze kukubaliana na mpango Wangu, bila kutonitii ama kuwa kigezo cha aibu Kwangu, na kuwa na ushuhuda unaovuma kwa sababu Yangu. Miongoni mwa wanadamu, kumekuwa na wale ambao Wamenitolea ushuhuda mzuri na kulipa jina Langu utukufu, lakini matendo ya mwanadamu, tabia ya mwanadamu vitawezaje kuutosheleza moyo Wangu? Atawezaje kufikia matakwa Yangu ama kutimiza mapenzi Yangu? Kwa milima yote na maji katika dunia, na maua, nyasi, na miti iliyo duniani, hapana hata moja isiyonyesha kazi ya mikono Yangu, hakuna hata moja isiyokuwepo kwa ajili ya jina Langu. Ilhali mbona mwanadamu hawezi kufikia kiwango kile Ninachohitaji? Je, inaweza kuwa kwa sababu ya hali yake ya chini mno? Je, inaweza kuwa ni kwa sababu ya kuinuliwa kwake na Mimi? Je, inaweza kuwa ni kwa sababu Mimi ni mkatili kwake? Mbona kila wakati mwanadamu ana hofu kwa sababu ya mahitaji Yangu? Leo, miongoni mwa wengi katika ufalme, ni kwa nini mnasikia tu sauti Yangu lakini hamtaki kuuona uso Wangu? Mbona mnayaangalia tu maneno Yangu bila kujaribu kuyalinganisha na Roho Wangu? Mbona mnanitofautisha juu mbinguni na chini duniani? Je, yawezekana kwamba Mimi, Nikiwa duniani, Siko sawa na Mimi niliye mbinguni? Je, yawezekana kwamba Mimi, Ninapokuwa mbinguni, Siwezi kushuka chini duniani? Je, yawezekana kwamba Mimi, Nikiwa duniani, Sistahili kuwa wa mbinguni? Ni kana kwamba Mimi, Ninapokuwa duniani, Mimi ni kiumbe duni, kana kwamba Mimi, Ninapokuwa mbinguni, Mimi ni kiumbe Aliyetukuzwa, na kama kwamba kuna shimo kubwa lisilopitika kati ya mbinguni na dunia. Lakini katika dunia ya wanadamu wanaonekana kutojua kitu chochote kuhusu asili ya vitu hivi, lakini wakati huo wote wamekuwa wakienda kinyume na Mimi, kana kwamba maneno Yangu yana sauti tu na hayana maana. Wanadamu wote wanaweka bidii kwa maneno Yangu, wakifanya uchunguzi wao kuhusu sura Yangu ya nje, lakini wote wanapata kushindwa, bila matokeo yoyote ya kuonyesha, badala yake, wanapigwa chini na maneno Yangu na hawawezi thubutu kusimama tena.

Nikiiweka imani ya binadamu katika majaribu, hakuna hata mwanadamu mmoja aliye na uwezo wa kuwa na ushuhuda wa kweli, hakuna hata mmoja anayeweza kujitoa kikamilifu; badala yake, mwanadamu anashinda akijificha na kukataa kujifungua na kuwa wazi, kana kwamba Ninaenda kuupora moyo wake. Hata Ayubu hakustahimili majaribu, wala hakufurahia katika mateso. Watu wote wanatoa dokezo iliyofifia ya kijani kibichi katika joto la majira ya kuchipua; wao hawasalii kwenye hali ya kijani kibichi chini ya mlipuko wa baridi wa majira ya

baridi. Akiwa mwenye mifupa na mkonde na gofu kwa kimo, mwanadamu hawezi kutimiza nia Zangu. Katika binadamu wote, hakuna hata mmoja anayeweza kutumika kuwa mfano kwa wengine, kwa sababu wanadamu ni sawa tu, bila tofauti kati yao, na kuna kidogo kinachowatofautisha mmoja na mwingine. Kwa sababu hii, hata leo wanadamu bado hawana uwezo wa kuijua kazi Yangu. Ni wakati ambao kuadibu Kwangu kutawashukia wanadamu ndipo wanadamu, bila kujua, wataifahamu kazi Yangu, na bila Mimi kufanya lolote ama kumlazimisha yeyote, wanadamu watakuja kunijua, na hivyo kupata kuiona kazi Yangu. Huu ni mpango Wangu, ni kipengele cha kazi Yangu ambayo ni wazi, na ni kile mwanadamu lazima afahamu. Katika ufalme, vitu vingi visivyohesabika vya uumbaji vinaanza kufufuka na kupata nguvu ya maisha yao. Kwa sababu ya mabadiliko katika hali ya dunia, mipaka kati ya nchi moja na nyingine pia inaanza kusonga. Hapo awali, Nimetabiri: Wakati ardhi itagawanywa kutoka kwa ardhi, na ardhi kujiunga na ardhi, huu ndio utakuwa wakati ambao Nitayapasua mataifa kuwa vipande vidogo. Katika wakati huu, Nitafanya upya uumbaji wote na kuugawa tena ulimwengu mzima, hivyo kuweka ulimwengu katika mpangilio, Nikibadilisha hali yake ya awali kuwa mpya. Huu ndio mpango Wangu. Hizi ni kazi Zangu. Wakati mataifa na watu wa dunia watakorudi mbele ya kiti Changu cha enzi, basi Nitachukua fadhila ya mbinguni na kuiweka kwa sababu ya ulimwengu wa binadamu, ili, kwa mujibu Wangu, itajazwa na fadhila isiyo ya kufananisha. Lakini ulimwengu wa kitambo ukiendelea kuwepo, Nitavurumisha hasira Yangu kwa mataifa yake, Nikieneza amri Zangu za utawala katika ulimwengu mzima, na kuleta kuadibu kwa yeyote anayezikiuka:

Ninapougeuza uso Wangu kwa ulimwengu kuzungumza, binadamu wote wanasikia sauti Yangu, na hapo kuona kazi yote ambayo Nimefanya katika ulimwengu. Wale wanaoenda kinyume na mapenzi Yangu, hivyo ni kusema, wanaonipinga kwa matendo ya mwanadamu, watapitia kuadibu Kwangu. Nitachukua nyota nyingi mbinguni na kuzitengeneza upya, na kwa mujibu Wangu jua na mwezi vitafanywa upya—anga hazitakuwa tena jinsi zilivyokuwa hapo awali; vitu visivyohesabika duniani vitafanywa kuwa vipya. Yote yatakuwa kamili kupitia maneno Yangu. Mataifa mengi katika ulimwengu yatagawanishwa upya na kubadilishwa kuwa taifa Langu, ili kwamba mataifa yote yaliyomo duniani yatatoweka milele na kuwa taifa linaloniabudu Mimi; mataifa yote ya dunia yataangamizwa, na hayatakuwepo tena. Kati ya binadamu walio ulimwenguni, wale wote walio wa Shetani wataangamizwa; wale wote wanaomwabudu Shetani watalazwa chini na moto Wangu unaochoma—yaani, isipokuwa wale walio ndani ya mkondo, waliobaki watabadilishwa kuwa jivu. Nitakapoadibu watu wengi, wale walio katika dunia ya kidini, kwa kiasi tofauti, watarudi kwa ufalme Wangu, wakiwa wameshindwa na kazi Yangu, kwani watakuwa wameona kufika kwa Aliye Mtakatifu akiwa amebewa juu ya wingu jeupe. Wanadamu wote watafuata aina yao, na watapokea kuadibu

kunakotofautiana kulingana na kile walichofanya. Wale ambao wamesimama kinyume na Mimi wataangamia; na kwa wale ambao matendo yao duniani hayakunihusisha, kwa sababu ya vile wamejiweka huru wenyewe, wataendelea kuwa duniani chini ya uongozi wa wana Wangu na watu Wangu. Nitajionyesha kwa mataifa mengi yasiyohesabika, Nikipaza sauti Yangu kote duniani Nikitangaza kukamilika kwa kazi Yangu kuu ili wanadamu wote waone kwa macho yao.

Sauti Yangu inapoimarika kwa uzito, pia Ninaichunguza hali ya ulimwengu. Kupitia kwa maneno Yangu, vitu visivyohesabika vya uumbaji vyote vinafanywa upya. Mbingu inabadilika, kama ifanyavyo dunia. Binadamu wanafunuliwa wakiwa katika hali yao halisi na, polepole, kila mtu anatengwa kulingana na aina yake, na kutafuta njia bila kujua wanajipata wakirejea katika ngome za familia zao. Hii itanifurahisha sana. Niko huru kutokana na vurugu, na bila kutambulika, kazi Yangu kuu inatimizwa, na vitu visivyohesabika vya uumbaji vinabadilishwa, bila kujua. Nilipoumba ulimwengu, Niliunda kila kitu kulingana na aina yake, Nikiweka vitu vyote vilivyo na maumbo pamoja na mifano zao. Wakati mpango wa usimamizi Wangu unapokaribia tamati, Nitarejesha hali ya awali ya uumbaji, Nitarejesha kila kitu kiwe katika hali ya awali, Nikibadilisha kila kitu kwa namna kubwa, ili kila kitu kirudi ndani ya mpango Wangu. Muda umewadia! Hatua ya mwisho katika mpango Wangu iko karibu kutimika. Ah, dunia ya kitambo yenye uchafu! Kwa hakika mtaanguka chini kwa maneno Yangu! Kwa hakika mtafanywa kuwa bure kwa mujibu wa mpango Wangu! Ah, vitu visivyohesabika vya uumbaji! Wote mtapata maisha mapya katika maneno Yangu—utapata uhuru wako Bwana Mkuu! Ah, dunia mpya, safi isiyo na uchafu! Kwa kweli mtafufuka katika utukufu Wangu! Ah Mlima Zayuni! Usiwe kimya tena. Nimerudi kwa ushindi! Kutoka miongoni mwa uumbaji, Ninaichunguza dunia nzima. Duniani, wanadamu wameanza maisha mapya, wameshinda tumaini mpya. Ah, watu Wangu! Mtakosaje kurudi kwa maisha ndani ya mwanga Wangu? Mtakosaje kuruka kwa furaha chini ya uongozi Wangu? Ardhi zinapiga kelele kwa furaha, maji yanapiga kelele kali na vicheko vya furaha! Ah, Israeli iliyofufuka! Mtakosaje kuhisi fahari kwa mujibu wa majaaaliwa Yangu? Ni nani amelia? Ni nani ameomboleza? Israeli ya kitambo haiko tena, na Israeli ya leo imeamka, imara na kama mnara, katika dunia, imesimama katika mioyo ya binadamu wote. Israeli ya leo kwa hakika itapata chanzo cha uwepo kupitia kwa watu Wangu! Ah, Misri yenye chuki! Hakika, bado hamsimami dhidi Yangu? Mnawezaje kuichukulia huruma Yangu kimzaha na kujaribu kuepuka kuadibu Kwangu? Mtakosaje kuwa katika kuadibu Kwangu? Wale wote ambao Nawapenda wataishi milele kwa hakika, na wale wote wanaosimama dhidi Yangu wataadhibiwa na Mimi milele kwa hakika. Kwani Mimi ni Mungu mwenye wivu, Sitawasamehe kwa urahisi wanadamu kwa kile watakachokuwa wametenda. Nitaingalia dunia yote, na, Nikitokea Mashariki ya dunia na haki, adhama, ghadhabu, na kuadibu, Nitajionyesha binafsi kwa wanadamu wengi wa tabaka mbalimbali!

Sura ya 27

Kamwe mienendo ya binadamu haijawahi kuugusa moyo Wangu, wala kuonekana Kwangu kama kitu cha thamani. Machoni mwa mwanadamu, daima Mimi huwa mkali kwake kila wakati, na kila mara Nimemweka chini ya mamlaka kali. Ndani ya matendo yote ya mwanadamu, ni mambo machache sana anayonifanyia Mimi, na mara nyingi hapana kitendo chake kisimamacho imara machoni Pangu. Hatimaye, kila kitu cha mwanadamu kinaanguka mbele Yangu bila mnong'ono; mwanadamu kimeporomoka polepole mbele Yangu, na ni katika nyakati kama hizi ndipo matendo Yangu hudhihirika, na kumfanya kila mmoja, katika upotovu wake, kunitambua Mimi. Hali ya mwanadamu haibadiliki kamwe. Kilicho ndani ya mioyo yao sio kulingana na mapenzi Yangu—sio Ninachohitaji. Jambo Ninalochukia zaidi ni ugumu na uhalifu sugu wa mwanadamu na ukaidi sugu, lakini ni nguvu zipi ambazo huwachochea wanadamu waendeleo kushindwa kunijua, kuwafanya waniweke mbali na wao kila mara, na kutotenda kulingana na mapenzi Yangu mbele Yangu kamwe lakini kunipinga nyuma Yangu? Je, huu ndio uaminifu wao? Huu ndio upendo wao Kwangu? Mbona wasitubu dhambi zao na kuzaliwa mara ya pili? Mbona binadamu hupenda kuishi kwenye chemichemi badala ya kuishi mahali pasipo na matope? Inawezekana kuwa Mimi Nimewadhulumu? Inawezekana kuwa Mimi Nimewapotosha? Inawezekana kuwa Mimi nimewaelekeza kuzimu? Kila mtu anataka kuishi “kuzimu.” Mwangaza unapotokea, macho yao hupofuka ghafla, kwa kuwa kila chao kinatoka kuzimu. Ilhali watu hawana ufahamu wa mambo haya na wanafurahia tu “raha za motoni.” Wao hata hushikilia kwa nguvu karibu na vifua vyao kama hazina wakihofu kwamba Mimi nitazinyakua hazina hizi, hivyo kuwaacha bila kiini cha kuwepo kwao. Wanadamu wananiogopa na ndio maana wao hukaa mbali na Mimi na kutokaa karibu Nami Ninapokuja duniani kwa maana “hawapendi kujiletea madhara,” wakiwa na ombi la kuishi maisha ya amani katika familia yao ili wawe na “maisha ya furaha duniani.” Lakini Siwezi kuruhusu wanadamu watende vile wanavyotaka, kwa kuwa lengo Langu hasa ni kuziangamiza familia zao. Kunzia wakati Nifikapo, amani inatoweka katika nyumba zao. Nakusudia kusambaratisha mataifa yote yatawanyike, sembuse familia ya mwanadamu. Ni nani awezaye kuepuka mkono Wangu? Itawezekanaje kuwa wale wanaopokea baraka wataepuka kwa sababu ya kutonuia kwao? Itawezekanaje kamwe kuwa wale walioadibiwa watapata huruma Yangu kwa sababu ya wao kuwa na woga? Katika maneno Yangu yote, wanadamu wameona mapenzi Yangu na kuona matendo Yangu, lakini ni nani awezaye kuondokana na minyororo ya mawazo yake mwenyewe? Ni nani anaweza kupata njia kutoka ndani au nje ya maneno Yangu?

Mwanadamu ameshuhudia upendo Wangu, mwanadamu amenitumikia kwa dhati, na

mwanadamu amenitii kwa kweli, akinifanyia kila kitu katika uwepo Wangu. Ilhali jambo hili haliwezi kutimizwa na watu ; wanalia tu katika roho zao kana kwamba wamenyakuliwa na mbweha mwenye njaa, na wanaweza tu kunitazama na macho yenye hamu, wakinililia bila kukoma. Lakini mwishowe, hawawezi kujiondoa katika matatizo yanayowakumba. Ninakumbuka jinsi ambavyo watu wa kale waliweka ahadi mbele Zangu, wakiapa kwa mbingu na dunia mbele Zangu kulipiza ukarimu Wangu kwa upendo. Walilia kwa uchungu mbele Yangu, na kilio chao kilikuwa cha kuvunja moyo, kigumu kuvumilia. Kwa sababu ya azimio lao, mara nyingi niliwapa watu msaada. Mara nyingi, wanadamu wamekuja mbele Zangu kunitii, mienendo yao ya kupendeza isiyoweza kusahaulika. Mara nyingi, wamenipenda bila kutikisika katika uaminifu wao, bidii yao ikiwa ya kupendeza. Mara nyingi, wamenipenda hadi kiwango cha kuhatarisha maisha yao, wakanipenda Mimi hata zaidi ya wanavyojipenda wenyewe—na kwa vile Nimeona upendo huu ni wa kweli, Nimeukubali. Mara nyingi, wamejitoa kama sadaka mbele Yangu, bila kujali mauti kwa sababu Yangu, na Nimepangusa wasiwasi huo nyusoni mwao, na kwa uangalifu nimekadiria maumbile yao. Kumekuwa na nyakati zisizohesabika ambapo Nimewapenda kama kitu kinachothaminiwa, na kuna wakati mwingine mwingi ambao Nimewachukia kama adui Zangu. Hata hivyo, kile kilicho fikirani Mwangu hakiwezi kueleweka na mwanadamu. Wanadamu wakiwa na huzuni, Mimi huja kuwafariji, na wakiwa wanyonge Mimi huja kuwasaidia katika mwendo. Wanapopotea njia, Mimi huwapa mwelekeo. Wanapolia, Mimi hufuta machozi yao. Lakini, Nionapo huzuni, nani anaweza kunifariji kwa moyo wake? Ninapopatwa na hofu, ni nani hujali hisia Zangu? Ninapooni huzuni, ni nani anayeweza kutibu kidonda kilicho moyoni Mwangu? Ninapohitaji mtu karibu Nami, ni nani anayejitolea kushirikiana na Mimi? Inawezekana kuwa malengo yao ya kale Kwangu yamebadilika yasiweze kurudi tena? Ni kwa nini kwamba hakuna lolote kati ya haya wanalokumbuka? Inawezekanaje kuwa wanadamu wameyasahau yote haya? Je, haya yote si kwa sababu ya mwanadamu kupotoshwa na adui yake?

Malaika wanapocheza muziki wakinisifu, hii inasisimua huruma kwa ajili ya binadamu. Moyo wangu unajawa na huzuni ghafla, na inakuwa vigumu kujiondoa katika hisia hii ya kuhuzunisha. Katika furaha na huzuni ya kutengana na kisha kuunganika Kwangu na mwanadamu, hatuwezi kubadilishana mawazo. Kwa sababu tumetengana mbinguni na wanadamu ardhini, nyakati ambapo Mimi na mwanadamu tunaweza kukutana ni nadra sana. Ni nani anayeweza kujitoa katika kuwaza mambo mazuri ya kale? Ni nani anayeweza kuzuia picha hizi za ukumbusho kumwonekana? Ni nani asingetumaini kuendelea kwa hisia hizi nzuri? Ni nani hangetamani kwa hamu kurudi Kwangu? Ni nani asingetamani sana kuunganishwa Kwangu na mwanadamu tena? Moyo Wangu una hofu nyingi, na nafsi ya binadamu imejaa wasiwasi mwingi. Licha ya sisi kuwa katika nafsi moja, hatuwezi kuwa pamoja mara kwa mara, na

hatuwezi kuonana mara kwa mara. Kwa sababu hii, maisha ya wanadamu wote yamepata pigo kuu na hayana nguzo za nguvu muhimu, kwa sababu wamekuwa na hamu kuu Kwangu. Ni kana kwamba wao ni viumbe waliorushwa kutoka mbinguni, wakiliita jina Langu kutoka duniani, wakiinua macho yao Kwangu kutoka ardhini—lakini wanawezaje kuepuka kutoka kwa midomo ya mbwa mwitu mlaifi? Wanawezaje kujiokoa kutokana na tishio na majaribu yake? Binadamu wanawezaje kukosa kujitolea kwa sababu ya kutii utaratibu wa mpango Wangu? Wanaponisihi kwa sauti, Ninageuza uso Wangu kutoka kwao, kwa maana Sitaki kushuhudia zaidi ya hayo; Lakini, itawezekanaje Nisisikie vilio vya watu hawa? Nitarekebisha udhalimu katika dunia ya mwanadamu. Nitafanya kazi Yangu kwa mikono Yangu mwenyewe ulimwenguni kote, Nikimkomesha Shetani asiwadhuru watu Wangu tena, Nikiwakataza maadui wasifanye kile wapendacho tena. Nitakuwa Mfalme duniani na kukipeleka kiti Changu cha enzi huko, na kuwafanya maadui Wangu wote waanguke chini na kukiri makosa yao mbele Yangu. Katika hali Yangu ya huzuni, hasira imechanganywa, Nitaुकanyaga ulimwengu wote sawasawa, bila kumwacha yeyote, na kuwatia maadui Wangu hofu kubwa. Naiangamiza dunia nzima, na kuwafanya maadui Wangu waanguke katika maangamizo hayo, ili kuanzia sasa na kuendelea wasiwapotoshe wanadamu tena. Mpango Wangu tayari umeamuliwa, na hakuna yeyote, haijalishi ni nani, atakayeubadilisha. Ninapotentembea kwa fahari kuu ulimwenguni, wanadamu wote watafanywa wapya, na kila kitu kitapewa uhai tena. Mwanadamu hataalia tena, hatanililia tena akitaka msaada. Hapo, moyo Wangu utajawa na furaha tele, na wanadamu Watanirudia kwa shangwe. Ulimwengu mzima, kutoka juu mpaka chini, utabubujikwa na nderemo ...

Leo hii, miongoni mwa mataifa ya ulimwengu, Ninaendeleza kazi Niliyokusudia kukamilisha. Ninamtembelea kila mmoja, Nikifanya kazi Yangu jinsi Nilivyopanga, na binadamu wote wanayagawanya mataifa mengine kulingana na mapenzi Yangu. Watu walio duniani wameweka mawazo yao kwa hatima zao wenyewe, kwa maana siku yenyewe hakika inakaribia na malaika wanacheza parapanda zao. Hakutakuwa na kuchelewa tena, na kila kiumbe ataanza kucheza kwa shangwe. Ni nani anayeweza kusongeza siku Yangu kwa uwezo wake? Inawezekana kiwe kiumbe cha duniani? Zinaweza kuwa nyota angani au malaika? Ninapotoa tamko la kuanza ukombozi wa wana wa Israeli, siku Yangu inawaelekea watu wote wa ulimwengu. Kila mwanadamu anahofia kurejea kwa taifa la Israeli. Israeli itakaporejea, hiyo itakuwa siku Yangu ya utukufu, na pia, itakuwa siku ambayo kila kitu kitabadilika na kuwa kipya. Hukumu ya haki inapoukaribia ulimwengu, watu wote watakuwa na woga na hofu, kwa maana ulimwengu wa mwanadamu haufahamu haki. Wakati ambapo Jua la haki litaonekana, Mashariki itaangazwa, kisha litaangaza ulimwenguni kote, likimfikia kila mtu. Iwapo mwanadamu atatenda haki Yangu, ni kitu gani kitakuwa cha kuogopesha. Watu Wangu wote

wanangoja siku ya kurudi Kwangu, wanatarajia kwa hamu siku Yangu. Wanangoja Mimi niwaadhibu wanadamu wote na kupanga hatima ya wanadamu katika wajibu Wangu kama Jua la haki. Ufalme Wangu unaenea katika ulimwengu mzima, na kiti Changu cha enzi kimenyakua mioyo ya mamia ya milioni nyingi za watu. Kwa usaidizi wa malaika wa mbinguni, utimilifu Wangu mkuu utakamilika hivi karibuni. Wanangu na watu Wangu wote wanangoja kwa hamu kurejea Kwangu, wakitarajia kuunganishwa Kwangu nao, tusije tukatengana tena. Itawezekanaje watu wote wa ufalme Wangu wasikimbie wakifurahiana kwa kuunganika pamoja na Mimi tena? Inawezekana huu uwe muungano usio na gharama yoyote iliyolipwa? Mimi Ninaheshimiwa machoni pa kila mtu, Ninadhihirika katika maneno ya kila mtu. Nitakaporejea, aidha, Nitashinda nguvu zote za adui. Wakati umewadia! Nitaianza kazi Yangu, Nitatawala miongoni mwa wanadamu! Tazama, Ninarejea! Ninaondoka! Hili ndilo kila mmoja anatarajia, ndilo kila mmoja anatumainia. Nitawaruhusu binadamu wote watazame kufika kwa siku Yangu na wote watakaribisha siku Yangu kwa furaha tele!

Aprili 2,1992

Sura ya 28

Nilipokuja kutoka Zayuni, vitu vyote vilikuwa vimenisubiri, na Niliporudi Zayuni, Nilisalimiwa na wanadamu wote. Nilipokuja na kwenda, hatua Zangu hazikuwahi zuiliwa na vitu vilivyokuwa na uadui Kwangu, na kwa hivyo kazi Yangu iliendelea kwa utaratibu. Leo, Ninapokuja miongoni mwa viumbe vyote, vitu vyote vinanisalimu kwa kimya, kwa uoga mkuu kuwa Nitaondoka tena na Niondoe usaidizi kwao. Vitu vyote vinafuata uongozi Wangu, na vyote vinaangalia upande ulioashiriwa na mkono Wangu. Maneno ya kinywa Changu yamefanya kamili viumbe vingi na kuwaadibu wana wengi wa uasi Kwa hivyo, wanadamu wote wanaangalia maneno Yangu kwa makini, na kusikiza kwa karibu maneno ya kinywa Changu, na wanaogopa sana kupitwa na fursa hii nzuri. Ni kwa sababu hii ndio kwamba Nimeendelea kuzungumza, ili kazi Yangu iendelezwe kwa haraka, na ili hali ya kufurahisha ije duniani mapema na kuponya maeneo ya ukiwa duniani. Ninapoangalia mawinguni ndipo mara tena Namrejelea mwanadamu; nchi zote zinajaa uhai mara moja, hamna vumbi tena hewani, na wala matope hayafuniki ardhi nzima tena. Macho Yangu yaangaza mbele mara moja, na kuwafanya watu wa nchi zote Kunitazama na kutafuta usalama Kwangu. Miongoni mwa watu wa dunia ya sasa—wakiwemo wote walioko katika nyumba Yangu—Ni nani wanaotafuta kwa kweli hifadhi Kwangu? Ni nani wanaotoa mioyo yao kwa ajili ya gharama ambayo Nimelipa? Ni nani amewahi kuishi katika nyumba Yangu kwa amani? Ni nani amewahi kujitolea kwa kweli mbele Zangu? Ninapotoa mahitaji Yangu kwa mwanadamu, anafunga “kijighala” chake mara moja. Ninapompata mwanadamu, mara moja yeye hufungua mdomo wake kuchukua mali Yangu

kichinichini, na katika moyo wake, mara nyingi hutetemeka, akiwa na uoga mwingi kuwa Nitalipiza kisasi. Kwa hivyo kinywa cha mwanadamu ni nusu wazi na nusu kimefungwa na hana uwezo wa kuufurahia kwa kweli utajiri Niliampa. Huwa Simlaani mwanadamu kwa urahisi, lakini kila mara hunishika mkono na kuniomba Nirudishe huruma juu yake; na ni wakati tu mwanadamu anaponisihi ndipo Ninapotoa “huruma” juu yake, na Ninampa maneno makali ya kinywa Changu, kiasi kwamba anashikwa na aibu mara moja, na kwa kuwa hana uwezo wa kupata “huruma” Yangu moja kwa moja, badala yake anawafanya wengine wampishie huruma hiyo. Wakati ameelewa maneno Yangu yote kwa undani, kimo cha mwanadamu kiko sawa na matakwa Yangu, na maombi yake yanazaa matunda, na sio bure au batili; Ninabariki maombi ya mwanadamu yaliyo ya kweli, na sio kujifanya.

Nimekuwa Nikifanya matendo na kuzungumza kwa miaka, ila mwanadamu hajawahi sikia maneno Ninayoyazungumza leo, na hajawahi onja adhama Yangu na hukumu Yangu. Hata ingawa watu fulani wa dunia za kale wamesikia kumbukumbu za ukuu Wangu, hakuna ambaye amegundua kwa kweli upana wa mali Yangu. Ingawa watu wa sasa wanasikia maneno kutoka kwa kinywa Changu, wamebaki wapumbavu kuhusu siri zilizoko kinywani Mwangu, na hivyo wanauchukulia mdomo Wangu kama utoaji wa mambo mema ya namna maalum. Watu wote wanatamani kupata kitu kutoka kwenye kinywa Changu. Kama ni siri za taifa, au siri za mbinguni, au mienendo ya ulimwengu wa kiroho, au hatima ya mwanadamu, watu wote wanatamani kupata vitu kama hivyo. Hivyo, kama Ningewakusanya watu pamoja na kuwasimulia “hadithi”, wangeamka mara moja kutoka “vitanda walimolazwa” na kusikiza njia Yangu. Vitu vingi vinakosekana ndani ya mwanadamu: Hahitaju tu “nyongeza ya lishe” bali “usaidizi wa kimawazo” na “usambazaji wa lishe ya kiroho”. Hii ndiyo inayokosekana kwa watu wote: huu ndio “ugonjwa” wa kila mwanadamu. Ninatoa uponyaji kwa ugonjwa wa mwanadamu ili matokeo bora yatimizwe, ili watu wote wawe na afya nzuri, na ili, kupitia uponyaji Wangu warejeele hali ya kawaida. Je, mnalichukia kwa kweli lile joka kuu jekundu? Mnalichukia kwa kweli? Mbona Nimewauliza mara nyingi? Mbona Nimewauliza swali hili, mara tena na tena? Kuna picha gani ya joka kuu jekundu katika mioyo yenu? Picha hiyo kwa kweli imeondolewa? Hamchukulii kwa kweli kama baba yenu? Watu wote wanafaa kuona nia Yangu katika maswali Yangu. Sio kuwafanya watu wawe na hasira, au kuchochea uasi kati ya mwanadamu, au ili mwanadamu agundue njia yake mwenyewe, bali ni kuwawezesha watu wote wajifungue kutoka kwa minyororo ya lile joka kuu jekundu. Ila mtu yeyote asiwe na wasiwasi. Yote yatakamilika na maneno Yangu; hakuna mwanadamu atakayekula, na hakuna mwanadamu anayeweza kufanya kazi ambayo Nitaifanya. Nitaifanya hewa ya nchi yote iwe safi na Nitatoa madoadoa yote ya mapepo duniani. Tayari Nimeanza, na Nitaanza hatua ya kwanza ya kazi Yangu ya kuadibu katika makazi ya joka kuu jekundu. Hivyo inaweza kuonekana kuwa kuadibu Kwangu

kumeifikia dunia nzima, na lile joka kuu jekundu na mapepo yote machafu yatashindwa kuepuka kuadibu Kwangu, kwa kuwa Ninaziangalia nchi zote. Kazi Yangu duniani itakapokamilika, hapo ndipo, kipindi cha hukumu Yangu kitakamilika, Nitamuadibu kirasmi lile joka kuu jekundu. Watu Wangu wataona kuadibu Kwangu kwa haki kwa lile joka kuu jekundu, watamwaga sifa mbele kwa sababu ya haki Yangu, na milele watalisifu jina Langu takatifu kwa sababu ya haki Yangu. Hivyo basi, mtatenda wajibu wenu kirasmi, na mtanisifu kirasmi kotekote katika nchi, milele na milele!

Kipindi cha hukumu kitakapofika kilele, Sitaharakisha kumaliza kazi Yangu, bali Nitajumuisha ndani ushahidi wa enzi ya kuadibu na kuruhusu ushahidi huo kuonekana na watu Wangu wote; na katika haya kutazaliwa matunda mengi zaidi. Ushahidi huu ndio njia ambayo kwayo Naliadibu lile joka kuu jekundu, na Nitafanya watu Wangu kuliona kwa macho yao ili wajue zaidi kuhusu tabia Yangu. Wakati watu Wangu wananifurahia ni wakati joka kuu jekundu linaadibiwa. Kuwafanya watu wa joka kubwa jekundu kusimama na kuliasi joka ndiyo nia Yangu, na ndiyo njia ambayo Ninawakamilisha watu Wangu, na ni nafasi nzuri ya watu Wangu wote kukua maishani. Mwezi unaong'aa unapochomoza, usiku mtulivu unaangamizwa mara moja. Ingawa mwezi umepasuka, mwanadamu yumo katika hali ya uchangamfu, na anakaa kwa utulivu chini ya mwangaza wa mwezi, akifurahia eneo la kupendeza chini ya mwangaza. Mwanadamu hawezi elezea hisia zake; ni kama ana matamano ya kuelekeza mawazo yake kwa wakati wa kale, ni kama anataka kuangalia mbele kwa mambo ya baadaye, ni kama anafurahia yanayojiri. Tabasamu linaonekana usoni mwake, na katika hali ya hewa ya kupendeza kunatokea harufu kavu; wakati upepo mwanana unapopuliza, mwanadamu anagundua harufu hiyo nzuri na anaonekana kuleweshwa nayo, akishindwa kujisimamisha. Huu ndio wakati haswa ambapo Mimi Mwenyewe Nimekuja miongoni mwa mwanadamu, na mwanadamu anahisi kwa hali ya juu harufu yenye uzuri tele, na kwa hivyo wanadamu wote wanaishi kati ya harufu hii. Niko na amani na mwanadamu, na mwanadamu anaishi kwa amani Nami, na hana uasi tena katika jinsi anavyonichukulia, Sipogoi tena upungufu wa mwanadamu, hakuna tena huzuni katika uso wa mwanadamu. Kifo hakitishii tena wanadamu wote. Leo, Naenda pamoja na mwanadamu katika enzi ya kuadibu, kuenda mbele pamoja na yeye upande kwa upande. Nafanya kazi Yangu, ambayo ni kusema, Naipiga fimbo Yangu chini miongoni mwa mwanadamu na inaanguka juu ya kile kilicho na uasi ndani ya mwanadamu. Katika macho ya mwanadamu, fimbo Yangu huonekana kuwa na nguvu spesheli: inaangukia wale wote ambao ni maadui Wangu na haiwasamehei kwa urahisi: miongoni mwa wale wote wanaonipinga, fimbo hiyo inafanya kazi yake ya kiasili; wale wote walioko mikononi Mwangu wanafanya wajibu wao kulingana na nia Yangu, na wala hawajawahi enda kinyume na matakwa Yangu au kubadilisha nia yao. Kutokana na hayo, maji yatanguruma, milima itaanguka, mito mikuu itatawanyika, mwanadamu

atabadilika, jua litakua na mwangaza mdogo, mwezi utakuwa na giza zaidi, mwanadamu hatakuwa tena na siku za kuishi kwa amani, hakutakuwa tena na wakati wa amani katika nchi, mbingu haitawahi tena kuwa shwari, na kimya na haitawahi tena kuendelea. Vitu vyote vitafanywa vipya na kurudia hali vilivyoonekana mwanzoni. Nyumba zote duniani zitasambaratishwa, na mataifa yote duniani yatagawanywa; siku za marudiano kati ya mke na mume zitapita, mama na mwanawe hawatakutana tena, hakutakuwa tena na kuja pamoja kwa baba na bintiye. Nitayaharibu yote yaliyokuwa duniani. Siwapi watu fursa ya kutoa hisia zao, kwani Mimi sina hisia, na Nimekua katika kuchukua hisia za watu kwa kiasi kikubwa. Ni kwa sababu ya hisia baina ya watu ndiposa Nimewekwa kando, na hivyo Nimekuwa “mwingine” machoni mwao; ni kwa sababu ya hisia kati ya binadamu ndiposa Nimesahaulika; ni kwa sababu ya hisia za mwanadamu ndipo anapochukua fursa ya kuchukua “dhamira” yake; ni kwa sababu ya hisia za mwanadamu ndiposa kila mara amekuwa mwoga wa kuadibu Kwangu; ni kwa sababu ya hisia za mwanadamu ndiposa ananiita mkosa haki na mdhulumu, na kusema kuwa Sisikizi hisia za mwanadamu Ninapofanya mambo Yangu. Je Nina mrithi duniani? Ni nani kamwe, kama Mimi, amewahi kufanya kazi usiku na mchana, bila kufikiria chakula au usingizi, kwa ajili ya mipangilio yangu yote ya usimamizi? Mwanadamu anawezaje kulinganishwa na Mungu? Anawezaje kuwa sambamba na Mungu? Inawezekanaje, Mungu, anayeumba, Awe sawa na mwanadamu, anayeumbwa? Ninawezaje kuishi na kufanya mambo pamoja na mwanadamu duniani? Nani anahofia moyo Wangu? Ni maombi ya mwanadamu? Wakati mmoja Nilikubali kujumuika na mwanadamu na kutembea pamoja na yeye—na ndio, hadi sasa mwanadamu anaishi chini ya ulinzi Wangu, lakini kutakuwa na siku ambapo mwanadamu atajitenga kutoka kwa ulinzi Wangu? Hata ingawa mwanadamu hajawahi kujibebesha nzigi kwa ajili ya moyo Wangu, nani anaweza kuendelea kuishi katika nchi isiyo na mwangaza? Ni kwa sababu tu ya baraka Zangu ndiposa mwanadamu ameishi mpaka leo.

Aprili 4, 1992

Sura ya 29

Siku hiyo ambayo vitu vyote vilifufuliwa, Nilikuja miongoni mwa wanadamu, na Nimeshinda naye kwa siku zilizokuwa za ajabu usiku na mchana. Ni katika hatua hii tu ndipo mwanadamu anaona wepesi Wangu wa kufikiwa, na vile uhusiano wake na Mimi unavyozidi kuwa mwingi, anaona baadhi ya kile Ninacho na Nilicho—na kwa sababu hii, anapata ufahamu kunihusu. Miongoni mwa watu wote, Ninainua kichwa Changu na kutazama, na wote wanania. Hata hivyo, wakati maafa yanaikumba dunia, wanakuwa na wasiwasi mara moja, na sura Yangu inatoweka kutoka katika nyoyo zao; wakishikwa na hofu kutokana na kufika kwa maafa, hawasikii kusihi Kwangu. Nimepita kati ya wanadamu kwa miaka mingi, lakini hajawahi

kufahamu hili, na hajawahi kunijua. Leo Namwambia hili kwa kinywa Changu mwenyewe, na kufanya watu wote waje mbele Yangu kupata kitu kutoka Kwangu, lakini bado wanaendelea kukaa mbali Nami, na hivyo basi hawanijui. Wakati nyayo Zangu zitaukanyaga ulimwengu mzima na hadi miisho ya dunia, mwanadamu ataanza kutafakari juu yake mwenyewe, na watu wote watakuja Kwangu na kusujudu mbele Zangu na kuniabudu. Hii itakuwa siku ya utukufu Wangu, siku ya kurudi Kwangu, na pia siku ya kuondoka Kwangu. Sasa, Nimeanza Kazi Yangu miongoni mwa watu wote, Nimeanza kirasmi, katika ulimwengu wote, ukamilishaji wa mpango Wangu wa usimamizi. Kuanzia sasa na kuendelea, wowote ambao si waangalifu wanastahili kutumbukizwa katikati ya kuadibu kusiko na huruma wakati wowote. Hii si kwa sababu Mimi sina utu, lakini ni hatua ya mpango Wangu wa usimamizi; zote lazima ziendeleo kulingana na hatua za Mpango Wangu, na hakuna mwanadamu anayeweza kubadili hali hii. Ninapoanza kirasmi Kazi Yangu, watu wote wanatembea kama Mimi hatua kwa hatua, kiasi kwamba watu katika ulimwengu wote wanakuwa katika hatua na Mimi, kuna “shangwe” ulimwengu mzima, na mwanadamu anaendelezwa mbele na Mimi. Kwa sababu hii, joka kubwa jekundu mwenyewe anachapwa na Mimi mpaka anakuwa katika hali ya kuchanganyikiwa na wazimu, na anahudumia Kazi Yangu, na, licha ya kutokuwa na nia, anashindwa kufuata tamaa zake mwenyewe, na kukosa njia nyingine ila kujiwasilisha kwa udhibiti Wangu. Katika mipango Yangu yote, joka kubwa jekundu ni foili^[a] Yangu, adui Wangu, na pia mtumishi Wangu; kwa hivyo, Sijawahi kushusha “mahitaji” Yangu kwake. Kwa hivyo, hatua ya mwisho ya kazi Yangu katika mwili inakamilika katika nyumba ya joka huyu. Kwa njia hii, joka kubwa jekundu anapata uwezo zaidi wa kunitumikia Mimi vizuri, kwa njia ambayo Mimi Nitamshinda na kukamilisha Mpango Wangu. Ninapofanya kazi, malaika wote wanaanzisha vita vya maamuzi na Mimi na kuamua kutimiza matakwa Yangu katika hatua ya mwisho, ili watu walio duniani wajitoe Kwangu kama malaika, na wasiwe na haja ya kunipinga Mimi, na wasifanye chochote ambacho kinaniasi. Hii ndio elimumwendo ya kazi Yangu kotekote katika ulimwengu.

Madhumuni na umuhimu wa kuwasili Kwangu miongoni mwa mwanadamu ni kuwaokoa wanadamu wote, kuwaleta watu wote katika nyumba Yangu, kuunganisha mbingu pamoja na ardhi, na kufanya mwanadamu kufikisha “ishara” kati ya mbingu na dunia, kwa maana hiyo ndiyo kazi asili ya mwanadamu. Wakati Nilimuumba mwanadamu, Nilifanya mambo yote yawe tayari kwa ajili ya mwanadamu, na baadaye, Mimi Nikamruhusu mwanadamu kupokea utajiri Niliompa kulingana na masharti Yangu. Ndio maana Nasema ni kwa uongozi Wangu ndio maana wanadamu wote wamefikia siku hii. Na haya yote ni Mpango Wangu. Miongoni mwa watu wote, idadi kubwa ya watu ipo chini ya ulinzi wa Upendo Wangu, na idadi kubwa inaishi chini ya kuadibu kwa chuki Yangu. Ingawa watu wote wanaomba Kwangu, bado hawana uwezo wa kubadili hali yao ya sasa; mara tu wamepoteza matumaini, wanaweza tu kuwacha hali asili

ichukue mkondo wake na kusitisha uasi Kwangu, kwa maana haya ndiyo yote yanayoweza kukamilishwa na mwanadamu. Inapokuja kwa hali ya maisha ya mwanadamu, mwanadamu bado hajakata maisha halisi, yeye bado hajaona kupita katika udhalimu, ukiwa, na hali duni ya dunia—na hivyo, kama haingekuwa ujio wa maafa, watu wengi bado wangekumbatia hali halisi ya dunia, na bado wangejishughulisha katika ladha ya “uzima.” Je, hii si hali halisi ya dunia? Je, hii si sauti ya wokovu Ninayonena kwa mwanadamu? Kwa nini, miongoni mwa wanadamu, hakuna kamwe aliyenipenda kwa kweli? Ni kwa nini mwanadamu ananipenda tu katikati ya kuadibu na majaribu, lakini hakuna mwanadamu Anayenipenda chini ya ulinzi Wangu? Mimi Nimetoa kuadibu Kwangu mara nyingi juu ya mwanadamu. Wao wanaiangalia, kisha wanaipuuza, na hawawezi kujifunza na kutafakari juu yake kwa wakati huu, na hivyo yote yanayokuja juu ya mwanadamu ni hukumu isiyo na huruma. Hii ni mojawapo tu ya mbinu Zangu za kazi, lakini bado ni kwa ajili ya kumbadili mwanadamu na kumfanya aweze kunipenda.

Mimi Natawala katika ufalme, na zaidi ya hapo, Ninatawala katika ulimwengu mzima; Mimi ni Mfalme wa ufalme na pia Mkuu wa ulimwengu. Kutoka wakati huu na kuendelea, Nitawakusanya wote wasio wateule na Nitaanza kufanya kazi Yangu katika mataifa, Na Nitatangaza amri Yangu ya utawala kwa ulimwengu mzima, ili kwa mafanikio Niweze kuingia katika hatua ifuatayo ya Kazi Yangu. Mimi nitatumia kuadibu ili kueneza kazi Yangu katika Mataifa, ambayo ni kusema, Nitatumia nguvu dhidi ya wale wote walio watu wa Mataifa. Kwa kawaida, kazi hii itafanyika kwa wakati mmoja na ile Kazi Yangu miongoni mwa wale waliochaguliwa. Wakati watu Wangu wanatawala na kushika madaraka duniani ndio pia itakuwa siku ambayo watu wote duniani watakuwa wameshindwa, na zaidi ya hayo, utakuwa wakati Wangu wa mapumziko—na hapo tu ndipo Nitawaonekana wale walioshindwa. Mimi huonekana kwa ufalme mtakatifu, na kujificha kutoka kwa nchi ya uchafu. Wote walioshindwa na kuwa watiifu mbele Yangu wana uwezo wa kuuona uso Wangu kwa macho yao wenyewe, na uwezo wa kusikia sauti Yangu kwa masikio yao wenyewe. Hii ni baraka ya wale waliozaliwa katika siku za mwisho, hii ni baraka Niliyoamua kabla, na hii haiwezi kubadilishwa na mwanadamu yeyote. Leo, Ninafanya kazi kwa namna hii kwa ajili ya kazi ya baadaye. Kazi Zangu zote zinahusiana, katika yote kuna wito na mwikio: Kamwe hakuna hatua yoyote iliyokoma kwa ghafla, na kamwe hakuna hatua yoyote iliyofanywa kwa kujitegemea kivyake. Je, hivi sivyo ilivyo? Je, kazi ya siku za nyuma siyo msingi wa kazi ya leo? Je, maneno ya zamani si utangulizi wa maneno leo? Je, hatua za zamani si asili ya hatua za leo? Wakati Ninafungua rasmi hati ya kukunjwa ndio wakati watu ulimwenguni kote wanaadibiwa, wakati watu wote duniani wanakabiliwa na majaribu, na ndicho kilele cha Kazi Yangu; watu wote wanaishi katika nchi bila mwanga, na watu wote wanaishi huku kukiwa na tishio la mazingira yao. Kwa maneno mengine, ni maisha ambayo mwanadamu hajawahi kupitia kutoka wakati wa uumbaji mpaka

siku ya leo, na hakuna yeyote katika enzi zote aliyeweza “kustarehe” na aina hii ya maisha, na hivyo Ninasema kwamba Ninafanya kazi ambayo haijawahi kufanyika mbeleni. Hii ndiyo hali halisi ya mambo, na hii ni maana ya ndani. Kwa sababu siku Yangu inakaribia kwa wanadamu wote, kwa sababu haionekani kuwa mbali, lakini iko mbele ya macho ya mwanadamu, ni nani asiyeweza kuwa na uoga kwa sababu ya jambo hili? Ni nani asiyekuwa na furaha katika hili? Mji mchafu wa Babeli hatimaye umefika mwisho wake; mwanadamu amekutana na dunia mpya kabisa, na mbingu na dunia zimebadilishwa na kufanywa mpya.

Wakati Najitokeza kwa mataifa yote na watu wote, mawingu meupe yanaenea angani na kunifunika. Na pia, ndege duniani wanaimba na kunichezea kwa shangwe, wakiangazia hali duniani, na hivyo kusababisha vitu vyote duniani kuwa hai, kusiwe tena na “kuwa vumbi” lakini badala yake kuishi katika hali ya uzima. Wakati Niko mawinguni, mwanadamu anatambua uso Wangu na macho Yangu kwa umbali, na kwa wakati huu yeye anahisi uoga kidogo. Katika siku za nyuma, yeye alisikia “kumbukumbu za kihistoria” kunihusu katika ngano, na matokeo yake ni kuwa anayo imani nusu na nusu shaka Kwangu. Yeye hajui Niliko Mimi, au ukubwa wa uso Wangu—je ni mpana kama bahari, au kama usio na mwisho kama malisho ya majani mabichi? Hakuna anayejua mambo haya. Ni wakati tu mwanadamu anapouona uso Wangu katika mawingu leo ndipo anapohisi kwamba Mimi wa hadithi ni wa kweli, na hivyo anakuwa na upendeleo zaidi Kwangu, na ni kwa sababu tu ya matendo Yangu ndio upendo wake Kwangu unazidi kuwa mkubwa kidogo. Lakini mwanadamu bado hanijui, na anaona tu sehemu moja Yangu katika mawingu. Baada ya hapo, Ninanyosha mikono Yangu na kuionyesha kwa mwanadamu. Mwanadamu anashangaa, na kufunika mdomo kwa mikono yake, akiwa na uoga kuwa Nitampiga chini kwa mkono Wangu, na hivyo anaongeza heshima kidogo kwa upendo wake. Mwanadamu anaweka macho yake juu ya kila hatua Yangu, akiwa na hofu kuu kuwa Nitampiga chini wakati yeye hayuko makini-lakini kutazamwa na mwanadamu hakunizuii Mimi, na Ninaendelea kufanya kazi iliyo mikononi Mwangu. Ni tu katika matendo yote Ninayofanya ndipo mwanadamu ana upendeleo fulani Kwangu, na hivyo hatua kwa hatua anakuja mbele Zangu kujiunga Nami. Wakati ukamilifu Wangu unafichuliwa kwa mwanadamu, mwanadamu atauona uso Wangu, na kutoka hapo Sitauficha au kujikinga kutoka kwa mwanadamu. Katika ulimwengu, Nitaonekana hadharani kwa watu wote, na walio nyama na damu wote wataona matendo Yangu yote. Wale wote ambao ni wa roho hakika wataishi kwa amani katika Nyumba Yangu, na bila shaka watafurahia baraka za ajabu pamoja na Mimi. Wale wote ambao Ninawajali hakika wataepuka kuadibu, na kwa hakika wataepuka maumivu ya roho na maumivu makali ya mwili. Mimi Nitaonekana hadharani kwa watu wote na kutawala na kutumia mamlaka, ili harufu ya maiti isisambae tena ulimwenguni; badala yake, manukato Yangu yataenea katika dunia nzima, kwa sababu siku Yangu inakaribia, mwanadamu anaamka, kila kitu kilicho duniani

kiko katika utaratibu, na siku za kunusurika kwa dunia hazipo tena, kwa maana Mimi Nimefika!

Aprili 6, 1992

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Sura ya 30

Kati ya binadamu, wakati mmoja Nilifanya muhtasari wa ukaidi na udhaifu wa mwanadamu, na hivyo Nilielewa udhaifu wa binadamu na Nikafahamu vema ukaidi wake. Kabla ya kuwasili kati ya binadamu, Nilikuwa nimekuja kuelewa kitambo furaha na huzuni kati ya binadamu—na kwa sababu ya hili, Ninaweza kufanya kile ambacho binadamu hawezi, na kusema kile ambacho binadamu hawezi, na Mimi hufanya hivyo kwa urahisi sana. Je, hii siyo tofauti kati ya Mimi na binadamu? Na hii siyo tofauti dhahiri? Yaweza kuwa kwamba kazi Yangu hutimizwa na watu wa mwili na damu? Inawezekana kwamba Mimi ni wa aina moja na viumbe vilivyoumbwa? Watu wameniweka katika tabaka la aina ya kufanana—na hii siyo kwa sababu hawanijui Mimi? Kwa nini, badala ya kuinuka juu zaidi kati ya binadamu, lazima Nijinyenyekeze? Kwa nini wanadamu huendelea kunikataa Mimi, kwa nini wanadamu hawawezi kulitangaza jina Langu? Kuna huzuni kubwa moyoni Mwangu, lakini watu wangewezaje kujua? Wangewezaje kuona? Kutochukulia kile kinachonisikitisha Mimi kama muhimu sana katika maisha yao kimewaacha watu wakiwa wametiwa bumbuwazi na kuchanganyikiwa, kama kwamba wamemeza tu dawa ya usingizi; Ninapowaita, wao huendelea tu kuota, na hiyo hakuna ambaye amewahi kufahamu matendo Yangu. Leo, watu wengi sana bado wamelala fofofu. Ni wakati tu ambapo wimbo wa ufalme husikika ndipo wao hufumbua macho yao yenye usingizi na kuhisi huzuni kidogo ndani ya mioyo yao. Wakati ambapo fimbo Yangu hugonga kati ya binadamu, wao bado husikiliza kidogo sana, kana kwamba majaliwa yao hayana thamani kama mchanga wa baharini. Ingawa wengi sana kati yao wana ufahamu fulani, bado hawajui umbali ambao hatua Zangu zimefika—kwani hawajaribu kuuelewa moyo Wangu, na hivyo hawajawahi kamwe kuweza kujinasua kutoka kwa utumwa wa Shetani. Mimi hutembea juu ya vitu vyote, na Huishi kati ya vitu vyote, na wakati huo huo, Mimi huchukua nafasi ya kati ndani ya mioyo ya watu wote. Kwa sababu hii, watu huniona Mimi kuwa tofauti, wakiadini kwamba Mimi ni wa ajabu, ama sivyo kwamba Mimi na kutokana na hilo, imani yao Kwangu huimarika kila siku. Wakati mmoja Nilijinyoosha katika mbingu ya tatu, Nikiwatazama watu wote na vitu vyote ulimwenguni. Wakati ambapo Mimi hulala, watu hutulia, wakiwa na hofu kabisa ya kusumbua pumziko Langu. Wakati ambapo Mimi huamka, wao huchangamshwa mara moja, kana kwamba wanafanya kazi ya kunipa Mimi furaha kabisa. Je, huu sio mtazamo wa watu walio duniani

Kwangu? Nani kati ya watu wa leo huniona Mimi mbinguni na duniani kama mmoja? Nani asiyeiniheshimu Mimi katika mbingu? Na nani hanidharau Mimi duniani? Kwa nini mwanadamu hunitenganisha Mimi kila mara? Kwa nini mwanadamu kila mara huwa na mitazamo miwili tofauti kunihusu Mimi? Je, Mungu aliyepata mwili aliye duniani si Mungu anayeamrisha vyote mbinguni? Je, Mimi Niliye mbinguni Siko duniani sasa? Kwa nini watu huniona Mimi lakini hawanijui Mimi? Kwa nini kuna umbali mkubwa hivyo kati ya mbingu na dunia? Je, mambo haya hayastahili kuchunguzwa kwa kina sana na mwanadamu?

Wakati ambapo Mimi hufanya kazi yangu, na katika nyakati ambazo Mimi hutamka sauti Yangu, watu kila mara hutamani kuongeza “ladha” kwayo, kana kwamba kunusa kwao ni kukali zaidi kuliko Kwangu, kana kwamba wao hupendelea ladha yenye nguvu, na kana kwamba Mimi Sifahamu kile ambacho mwanadamu huhitaji, na hivyo lazima “Nimsumbue” mwanadamu “kujaliza” kazi Yangu. Mimi Sififizi nguvu za uhalisi wa watu kwa makusudi, lakini Huwauliza wajitakase kutegemea msingi wa kunijua Mimi. Kwa sababu wao hukosa mengi sana, Napendekeza kwamba watumie juhudi zaidi kufidia upungufu wao ili kuuridhisha moyo Wangu. Watu walinijua Mimi wakati fulani katika dhana zao, lakini hawakufahamu hili kabisa, na hivyo utunzaji wao ulikuwa sawa na kuuchukulia mchanga kama dhahabu. Wakati ambapo Niliwakumbusha, waliachilia tu kwa sehemu ya hili, lakini badala ya kubadilisha sehemu iliyokuwa imeenda na vitu vya fedha na dhahabu, wameendelea kufurahia sehemu iliyo mikononi mwao ambayo bado inasalia—na kutokana na hili, wao kila mara huwa wanyenyekevu na wavumilivu mbele Yangu; hawana uwezo wa kutangamana na Mimi, kwani wana dhana nyingi sana. Hivyo, Niliamua kukamata chote ambacho mwanadamu anacho na alichio na kukivurumisha mbali sana, ili wote waweze kuishi na Mimi na wasiweze tena kuwa mbali na Mimi. Ni kwa sababu ya kazi Yangu ndio mwanadamu haelewei mapenzi Yangu. Wengine huamini kwamba Nitahitimisha kazi Yangu kwa mara ya pili na kuwatupa jehanamu. Wengine huamini Nitaanza mbinu mpya ya kunena, na wengi wao hutetemeka kwa woga: Wao huogopa kwamba Nitakamilisha kazi Yangu na kuwaacha bila mahali pa kwenda, na wao huogopa kabisa kwamba Nitawaacha mara nyingine. Kila mara watu hutumia dhana za zamani kutathmini kazi Yangu mpya. Nilisema kwamba watu hawakuwa wameelewa kamwe mbinu ambayo Mimi hufanyia kazi—je, wangejieleza vizuri wakati huu? Je, dhana za zamani za watu si silaha ambazo huharibu kazi Yangu? Ninaponena na watu, wao huhepa kukaza macho Kwangu kila mara, wakiogopa sana kwamba macho Yangu yatatua juu yao. Hivyo, wao huinamisha vichwa vyao, kana kwamba wanakubali ukaguzi kutoka Kwangu—na hili halisababishwi na dhana zao? Kwa nini Nimejinyenyekeza mpaka leo, lakini hakuna aliyewahi kufahamu? Ni lazima Nimwinamie mwanadamu? Nilikuja kutoka mbinguni hadi duniani, Nilishuka kutoka juu hadi mahali pa siri, na kuja kati ya binadamu na kufichua kila Nilicho nacho na Nilicho kwake. Maneno Yangu ni ya

kweli na yenye ari, mavumilivu na yenye huruma—lakini nani amewahi kuona kile Nilicho na Nilicho nacho? Bado Nimefichwa kwa mwanadamu? Kwa nini ni vigumu sana Kwangu kukutana na mwanadamu? Ni kwa sababu watu wana shughuli nyingi sana katika kazi zao? Je, ni kwa sababu Ninapuuza wajibu Wangu, na watu wote wana kusudia kufuatilia ufanisi?

Katika mawazo ya watu, Mungu ni Mungu, na Hawezi kushughulishwa kwa urahisi, ilhali mwanadamu ni mwanadamu, na hapaswi kuwa mpotovu kwa urahisi—lakini matendo ya watu bado hayawezi kuletwa mbele Yangu. Yawezekana kuwa matakwa Yangu ni ya juu sana? Yawezekana kuwa mwanadamu ni mdhaifu sana? Kwa nini kila mara watu huviangalia viwango ambavyo Mimi huhitaji kutoka mbali? Je, kweli haviwezi kufikiwa na mwanadamu? Matakwa Yangu yanapangwa kutegemea “katiba” ya watu, na kwa hiyo hayajawahi kuzidi kimo cha mwanadamu—lakini hata hivyo, watu husalia wasioweza kutimiza viwango ambavyo Mimi huhitaji. Mara nyingi mno Nimetorokwa kati ya binadamu, mara nyingi mno watu wamenitazama Mimi na macho ya kudhihaki, kana kwamba mwili Wangu umefunikwa kwa miiba na ni wa kuchukiza sana kwao, na hivyo watu hunichukia Mimi sana, na huamini kwamba Sina thamani. Kwa njia hii, Mimi husukumwa mbele na nyuma na mwanadamu. Mara nyingi mno watu wamenileta nyumbani kwa bei ya chini, na mara nyingi mno wameniuza Mimi kwa bei ya juu, na ni kwa sababu ya hili ndio Najikuta katika hali Niliyo ndani leo. Ni kana kwamba watu bado wananipangia Mimi njama; wengi wao bado wanataka kuniuza Mimi kwa faida ya mamia ya mamilioni ya dola, kwani mwanadamu hajawahi kunitunza Mimi. Ni kana kwamba Nimekuwa suluhisho kati ya watu, au silaha ya nyuklia ambayo wao hutumia kupigana kati ya wenyewe kwa wenyewe, au mapatano yaliyowekwa sahihi kati yao—na kutokana na hili, Mimi, kwa kifupi, Sina thamani kabisa moyoni mwa mwanadamu, Mimi ni chombo cha nyumbani kisicho cha muhimu. Lakini Simshutumu mwanadamu kwa sababu ya hili; Sifanyi chochote ila kumwokoza mwanadamu, na kila mara Nimekuwa mwenye huruma kwa mwanadamu.

Watu huamini kwamba Nitahisi starehe wakati ambapo Nitawatupa watu jehanamu, kana kwamba Nafanya maafikiano hasa na jehanamu, na kana kwamba Mimi ni aina fulani ya idara ambayo ina utaalamu wa kuwauza watu, kana kwamba Mimi ni mtaalamu katika kuwatapeli watu na Nitawauza kwa bei ya juu mara tu Nikiwa nao mikononi Mwangu. Vinywa vya watu havilisemi, lakini ndani ya mioyo yao hili ndilo wao huamini. Ingawa wote wananipenda Mimi, wao hufanya hivyo kisiri. Je, Nimelipa gharama kubwa hivyo na kutumia nyingi hivyo kupata kiasi kidogo hiki cha upendo kutoka kwao kama malipo? Watu ni walaghai, na Mimi kila mara huchukua nafasi ya anayelaghaiwa. Ni kama kwamba Mimi ni mkosa hila kabisa. Mara tu wakishaona udhaifu huu, wao huendelea kunilaghai. Maneno kutoka kinywani Mwangu hayakusudii kuwafisha watu au kubandika vitambulisho juu yao bila mpango maalum—hayo ni uhalisi wa mwanadamu. Labda baadhi ya maneno Yangu “hupita kiasi,” kwa hivyo basi Naweza

tu “kuomba” msamaha wa watu; kwa sababu Mimi sina “ustadi” katika lugha ya mwanadamu, mengi ya yale ambayo Mimi husema hayawezi kuridhisha matakwa ya watu. Labda baadhi ya maneno Yangu huipenya mioyo ya watu, kwa hiyo Naweza tu “kuomba” kwamba wawe wastahimilivu; kwa sababu Mimi si stadi wa falsafa ya kuishi kwa mwanadamu na si wa moja kwa moja katika njia Ninayozungumza, mengi ya maneno Yangu huleta aibu ndani ya watu. Labda baadhi ya maneno Yangu hukemea kiini cha ugonjwa wa watu na kufichua ugonjwa wao, na hivyo Mimi hushauri kutumia baadhi ya dawa Niliyokutayarishia, kwani Sina kusudi la kukuumiza na dawa hii haina athari. Labda baadhi ya maneno Yangu hayaonekani kuwa “yenye uhalisi,” lakini “Nawaomba” watu wasiwe na wasiwasi—Mimi si “hodari” wa mkono na mguu, kwa hiyo maneno Yangu hayajatekelezwa. Naomba kwamba watu “wanivumilie” Mimi. Je, maneno haya yanamsaidia mwanadamu? Natumaini kwamba watu watapata kitu kutoka kwa maneno haya, ili maneno Yangu yasiwe bure kila mara!

Aprili 9, 1992

Sura ya 31

Sijawahi kuwa na nafasi ndani ya mioyo ya watu. Ninapowatafuta watu kweli, wao hufunga na kubana macho yao na kupuuza matendo Yangu, kana kwamba yote Nifanyayo ni jaribio la kuwafurahisha, kutokana na hilo wao daima huchukizwa na matendo Yangu. Ni kana kwamba Nakosa kujitambua kokote: Mimi kila mara hujiringa mbele ya mwanadamu, kusababisha kughadhibishwa ndani ya mwanadamu, ambaye ni “mwadilifu na mwenye haki.” Lakini chini ya hali mbaya kama hizo, Mimi huvumilia, na kuendeleza kazi Yangu. Hivyo, Nasema kwamba Nimeonja ladha tamu, chachu, chungu, na kali za uzoefu wa binadamu, na kwamba Naja katika upepo na kuenda na mvua, kwamba Nimepitia mateso ya familia, Nimepitia milima na mabonde ya maisha, na Nimepitia uchungu wa kuondoka kutoka kwenye mwili. Hata hivyo, Nilipokuja duniani, badala ya kunikaribisha Mimi kwa sababu ya taabu Nilizokuwa Nimepitia kwa ajili yao, watu “kwa upole” walikataa makusudi Yangu mazuri. Ningekosaje kuumizwa na hili? Ningekosaje kusikitishwa. Yaweza kuwa kwamba Nilipata mwili ili yote yamalizike hivi? Kwa nini mwanadamu hanipendi Mimi? Kwa nini upendo Wangu umelipwa na chuki ya mwanadamu? Yaweza kuwa kwamba Natakiwa kuteseka kwa njia hii? Watu wametoa machozi ya huruma kwa sababu ya taabu Yangu duniani, na wameshutumu udhalimu wa msiba Wangu. Lakini ni nani amewahi kuujua kweli moyo Wangu? Ni nani anaweza daima kufahamu hisia Zangu? Mwanadamu wakati fulani alikuwa na upendo mkubwa Kwangu, na wakati fulani mara nyingi alinitamani sana katika ndoto zake—lakini ni vipi ambavyo watu wa duniani wangeweza kufahamu mapenzi Yangu mbinguni? Ingawa watu wakati fulani walifahamu hisia Zangu za huzuni, ni nani amewahi kuwa na huruma kwa ajili ya mateso Yangu kama mtesekaji mwenzi?

Yaweza kuwa kwamba dhamiri ya watu duniani inaweza kuisimua na kubadilisha moyo Wangu wenye huzuni? Je, watu duniani hawawezi kuniambia Mimi kuhusu taabu isiyosemeka ndani ya mioyo yao? Roho za watu na roho Mtakatifu zinategemeana, lakini kwa sababu ya vizuizi vya mwili, akili za watu “zilishindwa kuzuia hasira.” Wakati fulani Niliwakumbusha watu waje mbele Yangu—lakini miito Yangu haikuwasababisha watu kutimiza Nilichowaambia; wao walitazama tu angani, macho yakijaa machozi, kana kwamba walibeba taabu isiyosemeka, kana kwamba kulikuwa na kitu kilichowazuia. Hivyo, walishikana mikono yao na kuinama chini ya mbingu kwa maombi ya unyenyekevu Kwangu. Kwa kuwa Mimi ni mwenye huruma, Natoa baraka Zangu miongoni mwa binadamu, na kufumba na kufumbua, wakati wa majilio Yangu binafsi miongoni mwa binadamu hufika—lakini mwanadamu amesahau kitambo kiapo chake kwa Mbingu. Je, huu sio uasi kwelikweli wa mwanadamu? Kwa nini mwanadamu kila mara husumbuliwa na “usahaulifu”? Je, Nimemchoma kisu? Je, Nimeubwaga mwili wake? Namwambia mwanadamu kuhusu hisia zilizo ndani ya moyo Wangu, na kwa nini kila mara yeye huniepa? Katika kumbukumbu za watu, ni kana kwamba wamepoteza kitu fulani na hakiwezi kupatikana popote, lakini pia kana kwamba kumbukumbu zao si sahihi. Hivyo, watu daima husumbuliwa na usahaulifu katika maisha yao, na siku za maisha ya wanadamu wote ziko katika mchafukoge. Lakini hakuna anayesimamia hili, watu hawafanyi chochote ila kukandamizana, na kuuana, ambayo yamesababisha hali ya ushinde mkali leo, na kusababisha wote chini ya ulimwengu kuanguka ndani ya maji machafu na matope, bila nafasi yoyote ya wokovu.

Nilipokuja miongoni mwa watu wote ndio wakati hasa ambapo watu waligeuka kuwa waaminifu Kwangu. Wakati huu, joka kubwa jekundu lilianza pia kuweka mikono yake katili juu ya watu. Nilikubali “mwaliko,” na kuleta “barua ya mwaliko” kutoka kwa mwanadamu Nilipokuja “kuketi katika meza ya karamu” kati ya binadamu. Waliponiona Mimi, watu hawakunitilia maanani, kwani Sikujipamba na mavazi ya utajiri na Nilikuwa Nimeleta tu “kitambulisho” Changu kuketi mezani na mwanadamu. Hakukuwa na vipodozi vya bei ghali usoni Mwangu, hakukuwa na taji juu ya kichwa Changu, na miguuni Pangu Nilivaa tu jozi ya viatu vya kawaida vilivyotengenezwa nyumbani. Kilichowasikitisha watu sana kilikuwa ukosefu wa rangi ya midomo mdomoni Mwangu. Zaidi ya hayo, Sikuzungumza maneno ya heshima, na ulimi Wangu haukuwa kalamu ya mwandishi stadi; badala yake, kila mojawapo ya maneno Yangu lilipenya sehemu ya ndani kabisa ya moyo wa mwanadamu, ambalo liliwapa watu fikira “yenye kufaa” zaidi ya mdomo Wangu. Kuachilia huko kulitisha kwa watu kunipa Mimi “utendewaji maalum,” na hivyo walinitendea Mimi kama mwanakijiji wa kawaida kutoka mashambani ambaye hakuwa na ufahamu wa ulimwengu, wala hekima. Lakini watu walipotoa “zawadi za pesa,” watu bado hawakunichukulia kama mheshimiwa, lakini walikuja tu mbele Yangu bila heshima yoyote, wakitembea polepole wakiwa na hamaki. Mkono Wangu

uliponyoshwa, walistaajabishwa mara moja, wakapiga magoti, na wakatoa sauti kubwa. Walichukua “zawadi Zangu zote za fedha”. Kwa sababu kiwango kilikuwa kikubwa, walifikiria mara moja kwamba Mimi ni milionea na wakavua upesi mavazi yaliyoraruka kutoka kwa mwili Wangu bila idhini Yangu, wakayabadili na mavazi mapya—lakini hili halikunifurahisha. Kwa sababu Sikuzoea maisha rahisi kama hayo, na Nilidharau utendewaji huu wa “daraja la kwanza,” kwa sababu Nilikuwa mzaliwa wa nyumba takatifu, na, inaweza kusemwa, kwa sababu Nilizaliwa katika “umaskini,” Sikuzoea maisha ya anasa ambayo Nilitumikiwa kwa kila hali. Natamani tu kwamba watu waweze kufahamu hisia zilizo moyoni Mwangu, kwamba waweze kustahimili taabu kidogo ili kukubali ukweli usiostarehesha kutoka kwa mdomo Wangu. Kwa sababu Sijawahi kamwe kuzungumza kuhusu nadharia, au kuweza kutumia siri za watu za kujuana ili kushirikiana nao, na kwa sababu Siwezi kurekebisha maneno Yangu kulingana na sura za watu au saikolojia yao, watu kila mara wamenichukia sana, wameamini Sistahili mwingiliano, na wamesema kwamba Nina ulimi wa upanga na kila mara huwaumiza watu. Lakini sina uwezo wa kuchagua: Wakati fulani “Nilichunguza” saikolojia ya mwanadamu, wakati fulani “Niliiga” falsafa ya maisha ya mwanadamu, na wakati fulani Nilienda katika “chuo cha lugha” kujifunza lugha ya mwanadamu, ili Niweze kupata ujuzi wa njia ambazo kwazo watu huzungumza, na kunena kama inavyofaa sura zao—lakini ingawa Nilitumia juhudi nyingi, na kuwatembelea “wataalam” wengi, yote yalikuwa bure. Hakujawahi kuwa na chochote cha ubinadamu ndani Yangu. Kwa miaka hii yote, juhudi Zangu hazijawahi kutoa matokeo hata kidogo, Sijawahi kuwa na welekevu hata kidogo katika lugha ya mwanadamu. Hivyo, maneno ya mwanadamu kwamba “kazi ngumu hufidia” “yanaakisiwa” na Mimi, na kutokana na hilo, maneno haya hufikia mwisho duniani. Bila watu kutambua, methali hii haijakubalika na Mungu atokaye mbinguni, kuthibitisha ya kutosha kwamba maneno kama haya ni yasiyothibitika. Hivyo Naomba msamaha kwa mwanadamu, lakini hakuna cha kufanywa—nani alinifanya Mimi kuwa “mjinga” hivi? Sina uwezo wa kujifunza lugha ya mwanadamu, wa kuwa bingwa katika falsafa ya maisha, wa kujuana na watu. Mimi huwashauri tu watu wawe wavumilivu, wafiche hasira iliyo ndani ya mioyo yao, wasijiumize kwa sababu Yangu. Nani alitufanya tuingiliane wenyewe kwa wenyewe? Nani alitufanya tukutane wakati huu? Nani alitufanya tuwe na maadili ya ushirikiano?

Tabia Yangu inajumuisha maneno Yangu yote, lakini watu hawawezi kuifahamu katika maneno Yangu. Wao hubishana tu juu ya tofauti ndogondogo kuhusu kile Nisemacho—na hiyo ina maana gani? Je, dhana zao kunihusu Mimi zinaweza kuwafanya wakamilifu? Je, vitu duniani vingeweza kutimiza mapenzi Yangu? Niliendelea kujaribu kuwafunza watu jinsi ya kuzungumza maneno Yangu, lakini ilikuwa kana kwamba mwanadamu alikuwa bubu, na hangeweza kamwe kujifunza namna ya kuzungumza maneno Yangu jinsi Ningetaka. Nilimfunza kinywa kwa

kinywa, lakini hajawahi kamwe kuweza kujifunza. Ni baada ya hili tu ndipo Nilifanya ugunduzi mpya. Watu wa dunia wangepotea kuzungumza maneno ya mbinguni? Je, hili halikiuki utaratibu wa jambo la asili? Lakini, kwa sababu ya ari na uchunguzi wa watu Kwangu, Nilianzisha sehemu nyingine ya kazi kwa mwanadamu. Sijawahi mwaibisha mwanadamu kwa sababu ya kasoro zake, lakini badala yake humpa mwanadamu kwa mujibu wa kile anachokosa. Ni kwa sababu ya hili tu ndiyo watu wana fikira zenye kufaa kidogo Kwangu, na Natumia nafasi hii kuwakusanya watu pamoja mara nyingine, ili waweze kufurahia sehemu nyingine ya utajiri Wangu. Wakati huu, watu kwa mara nyingine wamezamishwa katika furaha, uchangamfu na kicheko wakifuata upepo kandokando ya mawingu ya rangi nyeupe angani. Naufungua moyo wa mwanadamu, na mwanadamu mara moja ana uchangamfu mpya, na hayuko radhi kujificha kutoka Kwangu tena, kwa kuwa ameonja ladha tamu ya asali, na kwa hiyo analeta takataka yake yote kubadilishwa—kana kwamba Nimegeuka kuwa mahali pa kukusanyia takataka, au kituo cha kusimamia takataka. Hivyo, baada ya kuona “matangazo” yaliyobandikwa, watu huja mbele Yangu na kushiriki kwa hamu, kwa kuwa wao huonekana kufikiria kwamba wanaweza kupata “hedaya” chache, hivyo wote hunitumia “barua,” ili waweze kushiriki katika matukio Niliyoanzisha. Wakati huu hawaogopi hasara, kwa sababu “mtaji” wa shughuli hizi si mkuu, na hivyo wanathubutu kubahatisha kushiriki. Kama hakungekuwa na hedaya za kupatikana kwa kushiriki, watu wangeondoka uwanjani na kuuliza warudishiwe pesa zao, na wangehesabu pia “riba” wanayonidai. Ni kwa sababu viwango vya leo vya maisha vimeongezeka, kufikia “kiwango cha wastani cha ufanisi” na kutimiza “usasa,” na “watu wa kada ya juu” binafsi “wakienda mashambani” kupanga kazi, kwamba imani ya watu mara moja imezidisha mara nyingi—na kwa sababu “katiba” yao inageuka kuwa bora zaidi na zaidi, wao hunitazama Mimi kwa uvutiwaji, na wako radhi kufungamana na Mimi ili wapate imani Yangu.

Aprili 11, 1992

Sura ya 32

Watu wanapokusanyika pamoja na Mimi, moyo Wangu unajawa na furaha. Mara moja, Ninatoa baraka zilizo mkononi Mwangu miongoni mwa binadamu, ili watu waweze kukusanyika kwa mkutano na Mimi, na kutokuwa maadui wanaoniasi lakini marafiki wanaotangamana na Mimi. Hivyo, Mimi pia ni wa dhati kwa mwanadamu. Katika kazi Yangu, mwanadamu anaonekana kama mwanachama wa shirika la ngazi ya juu, hivyo Ninamzingatia zaidi, kwa maana daima amekuwa kusudi la kazi Yangu. Nimeweka imara mahali Pangu katika mioyo ya watu, ili mioyo yao iweze kuniheshimu—ilhali wanabaki wasiojua kabisa kwa nini Ninafanya hili, na hawafanyi lolote ila kusubiri. Ingawa kuna mahali ambapo Nimeweka imara katika mioyo ya watu, hawahitaji kwamba Niishi hapo. Badala yake, wanamsubiri “Mtakatifu” katika

mioyo yao kuwasili ghafla. Kwa sababu utambulisho Wangu ni duni sana, Sifikii mahitaji ya watu na hivyo Naondolewa na wao. Kwa sababu wanachotaka ni “Mimi” ambaye ni mwenye majivuno sana—ilhali Ninapokuja, Sikuonekana kwa njia hii kwa mwanadamu, kwa hivyo aliendelea kuangalia mbali, akimsubiri aliye moyoni mwake. Ninapokuja mbele ya watu, wananikataa mbele ya umma. Ningeweza tu kusimama upande mmoja, Nikisubiri “kushughulikiwa” na binadamu, Nikitazama kuona kile watu wangeishia kufanya na Mimi, hii “bidhaa” pungufu. Siyaangalii makovu ya watu, lakini katika sehemu yao ambayo haina makovu, na kutokana na hili Napata uridhisho. Katika macho ya watu, Mimi ni “nyota ndogo” tu ambayo imeshuka kutoka kwenye anga, Mimi ni mdogo zaidi tu mbinguni, na ujaji Wangu duniani leo uliagizwa na Mungu. Kwa hiyo, watu wamebuni fasiri zaidi za maneno “Mimi” na “Mungu,” wakiogopa sana kumzingatia Mungu pamoja na Mimi kuwa kitu kimoja. Kwa sababu taswira Yangu haina sura ya Mungu hata kidogo, watu wote wanaamini kwamba Mimi ni mtumishi ambaye si wa jamii ya Mungu, na kusema kwamba hii si taswira ya Mungu. Pengine kuna watu ambao wamemwona Mungu—lakini kwa sababu ya ukosefu Wangu wa utambuzi ulimwenguni, Mungu hajawahi “kuonekana” Kwangu. Pengine nina “imani” ndogo sana na hivyo watu wananiona kama aliye duni. Watu wanadhani kwamba iwapo mtu kweli ni Mungu, basi hakika atakuwa stadi katika lugha ya mwanadamu, kwani Mungu ndiye Muumba. Lakini ukweli ni kinyume kabisa: Mimi si bingwa tu katika lugha ya mwanadamu, lakini kuna nyakati ambazo Siwezi hata “kukimu” “upungufu” wake. Kwa hiyo, Nahisi kuwa “mwenye hatia” kidogo, kwani Sitendi jinsi watu “wanataka,” lakini Naandaa tu nyenzo na kufanya kazi kwa mujibu wa kile “wanachokosa.” Madai ninayofanya kutoka kwa mwanadamu si makubwa hata kidogo, lakini watu wanaamini vinginevyo. Hivyo, “unyenyekevu” wao unafichuliwa katika kila tendo lao. Daima wanastahili kuja mbele Yangu, wakiniongoza njia, wakiwa na hofu kubwa kwamba Nitapotea, wakiogopa kwamba Nitazurura katika misitu ya kale ndani ya milima. Kwa hiyo, watu daima wameniongoza mbele, wakiwa na hofu sana kwamba Nitaingia katika gereza la chini ya ardhi. Nina “wazo wa kufaa” kidogo kuhusu imani ya watu, kwa maana wamefanya kazi kwa bidii kwa ajili Yangu bila kufikiria chakula au usingizi, kiasi kwamba juhudi zao kwa ajili Yangu zimewaacha bila usingizi mchana na usiku na hata kuzeeka—ambalo linatosha kuonyesha kwamba imani yao “imevuka mipaka” ya ulimwengu, na “kuwapita” mitume na manabii kotekote katika enzi.

Sipigi makofi kwa raha kwa sababu ya ujuzi mkuu wa watu, wala Siwatazami kwa dharau kwa sababu ya upungufu wao. Nafanya tu kile kilicho mikononi Mwangu, Simtendei yeyote kwa njia ya pekee, lakini Nafanya tu kazi kulingana na mpango Wangu. Lakini watu hawajui mapenzi Yangu na wanaendelea kuombea vitu kutoka Kwangu, kana kwamba utajiri Niliowapa hauwezi kukidhi mahitaji yao, kana kwamba mahitaji yanashinda ugavi. Lakini katika enzi ya leo, watu

wote wanahisi kuna “kupanda kwa gharama za maisha”—na hivyo, wanashughulika sana na kile Nilichowapa wafurahie. Ni kwa sababu ya hili ndio wanachoshwa na Mimi, na hivyo maisha yao yanajaa vurugu, na hawajui kile wanachopaswa na wasichopaswa kula. Wengine hata hushika vitu ambavyo Nimewapa kufurahia, wakivitazama kwa makini. Kwa sababu watu walikuwa wanateseka kutokana na njaa, na si jambo rahisi kwao kupata furaha za leo, wote ni “wenye shukrani zisizokuwa na mwisho,” na kumekuwa na mabadiliko fulani katika mtazamo wao Kwangu. Wanaendelea kulia mbele Yangu; kwa sababu Nimewapa mengi sana, mbele Yangu wanaendelea kuushika mkono Wangu na kutoa “sauti za shukrani.” Natembea juu ya ulimwengu, na Ninapotentemba Ninawaangalia kwa makini watu wa ulimwengu mzima. Kati ya umati wa watu duniani, hakujawahi kuwa na wowote ambao wanafaa kwa kazi Yangu ama ambao wananipenda kwa kweli. Hivyo, kwa wakati huu Nahema kwa kuvunjika moyo, na watu wanatawanyika mara moja, wasikusanyike tena, wakiogopa sana kwamba “Nitawakamata wote katika wavu mmoja.” Ninatumia fursa hii kuja miongoni mwa wanadamu, kufanya kazi Yangu—kazi inayofaa—miongoni mwa watu hawa waliotawanyika, Nikiwachagua wale ambao wanafaa kufanyia kazi ndani yao. Sitaki “kuwazuia” watu katikati ya kuadibu Kwangu, wasitoroke kamwe. Nafanya tu kazi ambayo lazima Niifanye. Nimekuja kuomba “msaada” kutoka kwa mwanadamu; kwa sababu usimamizi Wangu unakosa matendo ya mwanadamu, haiwezekani kuimaliza kazi Yangu kwa ufanisi, jambo ambalo linaizuia kazi Yangu kuendelea mbele kwa ufanisi. Natumaini tu kwamba watu wana azimio la kushirikiana na Mimi. Siulizi kwamba wanipikie chakula kizuri, au wanipangie mahali pa kufaa ili Nilaze kichwa Changu, au wanitengenezee nguo za kupendeza—Siheshimu vitu hivi hata kidogo. Watu wanapoweza kuelewa mapenzi Yangu na kuendelea mbele na Mimi, bega kwa bega, Nitaridhika moyoni Mwangu.

Ni nani duniani amewahi kunipokea kwa moyo wake? Nani amewahi kunipenda na moyo wake? Upendo wa watu daima umezimuliwa, hata Mimi “sijui” mbona upendo wao hauwezi kuwa uliokauka na usiozimuliwa. Hivyo, pia kuna “mafumbo” mengi yaliyo ndani ya mwanadamu. Miongoni mwa viumbe vilivyoumbwa, mwanadamu anaonekana kama yule ambaye ni “wa muujiza” na “asiyeeleweka,” na hivyo ana “sifa” mbele Yangu, kana kwamba yeye ni wa hadhi sawa na Mimi—lakini haoni chochote kigeni kuhusu hii “hadhi” yake. Katika hili, si kwamba Siwaruhusu watu kuwa katika nafasi hii na kuifurahia, lakini kwamba Nataka wao wawe na hisia ya adabu, kwa wao kutojitukuza sana; kuna umbali kati ya mbingu na dunia, sembuse kati ya Mungu na mwanadamu. Je, hakuna hata umbali mkubwa zaidi kati yao? Duniani, mwanadamu na Mimi tuko “katika hali ileile,” na sisi “huvumilia hali mbaya pamoja.” Utambulisho Wangu haunisamehe kutopitia taabu ya dunia ya mwanadamu, na ni kwa sababu ya hili ndio leo Nimetumbukia katika hali hii. Sijawahi kuwa na mahali pa kuishi kwa amani

duniani, ndiyo sababu watu husema, “Mwana wa Adamu hajawahi kuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake.” Kwa hiyo, watu pia wamelia machozi ya huruma kwa ajili Yangu na kuweka kando yuan kumi kadhaa kwa ajili ya “mfuko wa msaada” kwa ajili Yangu. Ni kwa sababu ya hili tu ndio Nina mahali pa kupumzika; kama haingekuwa kwa “msaada” wa watu, nani ajuaye Ningeishia wapi!

Kazi Yangu itakapomalizika, Sitatafuta tena “msaada wa kifedha” kutoka kwa mwanadamu; badala yake, Nitatekeleza kazi Yangu ya asili, na Nitashusha “vitu vyote vya nyumba Yangu” kwa watu ili wavifurahie. Leo, kila mtu anajaribiwa katikati ya majaribu Yangu. Mkono wangu unapokuja kirasmi juu ya mwanadamu, watu hawatanitazama tena kwa macho ya kuvutiwa, lakini watanitendea na chuki, na wakati huu Nitaitoa mioyo yao mara moja ili wawe kielelezo. Ninauchunguza moyo wa mwanadamu chini ya “hadubini”—hakuna upendo wa kweli Kwangu hapo. Kwa miaka, watu wamekuwa wakinidanganya na kunipumbaza—inaonekana kuwa upande wa kushoto wa juu wa moyo na upande wa chini wa kushoto wa moyo zote zina sumu ya chuki Kwangu, na haishangazi, basi, kwamba Nina mtazamo kama huo kwao. Na bado wanabaki wasiojua kabisa kuhusu hili, wala hawalikiri. Niwaonyeshapo matokeo ya uchunguzi Wangu, bado hawaamki; ni kana kwamba, katika akili zao, haya yote ni mambo ya kale, na hayapaswi kutajwa tena leo. Hivyo, watu wanatazama tu “matokeo ya maabara” kwa kutojali. Wanarudisha karatasi na kutoweka kwa haraka. Zaidi ya hayo, wanasema mambo kama, “Haya si muhimu, hayana athari yoyote kwa afya yangu.” Wanatoa tabasamu ndogo ya dharau, na kisha kuna mtazamo unaotisha kidogo katika macho yao, kana kwamba wakidokeza kwamba Sifai kamwe kuwa mwadilifu sana, kwamba lazima Niwe mzembe zaidi. Ni kana kwamba ufunuo Wangu wa siri zao za ndani umevunja “sheria” za mwanadamu, na hivyo wanakuwa na chuki zaidi Kwangu. Hapo tu ndipo Mimi huona chanzo cha chuki ya watu. Hii ni kwa sababu Ninapotazama, damu yao inatiririka, na baada ya kupita kwa ateri katika miili yao inaingia moyoni, na ni wakati huu tu ndipo Mimi huwa na “ugunduzi” mpya. Ilhali watu hawafikiri chochote kuhusu hili. Wao ni wazembe kabisa, hawafikiri kile wanachopata au kupoteza, ambalo linatosha kuonyesha roho yao ya ibada “isiyo na ubinafsi.” Hawafikirii hali ya afya yao wenyewe, na “kurupuka hapa na pale” kwa ajili Yangu. Huu pia ni “uaminifu” wao na kile “kinachostahili kusifiwa” kuwahusu, kwa hivyo kwa mara nyingine Ninatuma barua ya “sifa” kwao, kwamba waweze kufurahishwa na hili. Lakini wanaposoma “barua” hii, mara moja wanahisi kukerwa kidogo, kwa maana yote wanayofanya kimekatajiwa na barua Yangu ya kimya. Daima Nimewaelekeza watu watendavyo, ilhali inaonekana wanachukia sana maneno Yangu; hivyo, punde tu Ninapofungua mdomo Wangu, wanafumba na kubana macho yao na kufunika masikio yao kwa mikono yao. Hawanitazami kwa heshima kwa sababu ya upendo Wangu, lakini daima wamenichukia, kwa maana Nilionyesha upungufu wao, Nikifunua bidhaa

zote wanazomiliki, na hivyo basi wamegubikwa na hasara katika biashara yao, na riziki yao imetoweka. Hivyo, chuki yao Kwangu inaongezeka kutokana na hiyo.

Aprili 14, 1992

Sura ya 33

Katika nyumba Yangu, kulikuwapo wakati mmoja wale waliolisifu jina Langu takatifu, ambao walifanya kazi bila kuchoka ili utukufu Wangu duniani ungejaza anga. Kwa sababu ya hili, Nilifurahi sana, moyo Wangu ulijawa na furaha—lakini nani angeweza kufanya kazi badala Yangu, akiacha usingizi usiku na mchana? Azimio la mwanadamu mbele Yangu hunipa raha, lakini uasi wake huchochea hasira Yangu, na hivyo, kwa sababu mwanadamu hawezi kamwe kuzingatia wajibu wake, huzuni Yangu kwa ajili yake inakua kubwa zaidi. Kwa nini watu daima hawawezi kujitolea Kwangu? Kwa nini daima wao hujaribu kubishana na Mimi? Mimi ni msimamizi mkuu wa kituo cha biashara? Kwa nini Mimi hutimiza kwa moyo kamili kile ambacho watu hudai kutoka Kwangu, lakini Nitakacho kutoka kwa mwanadamu hakitimii? Inawezekana kuwa mimi Sina maarifa katika njia za biashara, lakini mwanadamu anayo? Kwa nini watu daima hunidanganya kwa mazungumzo ya ushawishi na ya kusifu mno? Kwa nini watu kila mara huja wakibeba “zawadi,” wakiomba njia ya kurudi ndani? Je, hili ndilo Nililomfundisha mwanadamu kufanya? Kwa nini watu hufanya mambo hayo haraka na kwa unadhifu? Kwa nini watu kila mara huhamasishwa kunidanganya? Ninapokuwa kati ya wanadamu, watu hunitazama kama kiumbe aliyeumbwa; Ninapokuwa katika mbingu ya tatu, wananiona kama Mwenyezi, Anayetawala vitu vyote; wakati Niko angani, wananiona kama Roho ambaye hujaza vitu vyote. Kwa jumla, hakuna mahali panaponistahili katika mioyo ya watu. Ni kama kwamba Mimi ni mgeni asiyekaribishwa, watu wananichukia sana, na hivyo wakati Ninachukua tiketi na kuchukua kiti Changu, wananifukuza nje, na kusema kwamba hakuna mahali pa Mimi kukaa hapa, kwamba Nimekuja mahali pabaya, na hivyo sina budi ila kuondoka kwa nguvu. Ninaamua kutoshirikiana na mwanadamu tena, kwa kuwa watu wana akili finyu, ukarimu wao ni haba sana. Sitakula kwenye meza moja nao tena, Sitazungumza nao tena duniani. Lakini Ninapozungumza, watu wanashangaa, wanaogopa kwamba Nitaondoka, na kwa hiyo wanaendelea kunikawisha. Nionapo upendo wao, mara moja Nahisi huzuni na upweke ndani ya moyo Wangu kwa kiasi fulani. Watu wanaogopa kwamba Nitawaacha, na hivyo wakati Ninapoachana nao, sauti ya kilio hujaza nchi, na nyuso za watu hufunikwa kwa machozi. Nafuta machozi yao, Nawainua juu tena, na wananitazama Mimi, macho yao ya kusihi inavyoonekana kwa nje ikiniomba Nisiende, na kwa sababu ya “unyofu” wao Niko nao. Lakini ni nani anayeweza kuelewa maumivu yaliyo ndani ya moyo Wangu? Ni nani anayezingatia mambo Yangu yasiyoelezeka? Kwa macho ya watu, ni kama kwamba Sina hisia, na hivyo daima

tumekuwa katika familia mbili tofauti. Wangewezaje kuona hisia ya huzuni ndani ya moyo Wangu? Watu hutamani tu raha zao wenyewe, na hawajali mapenzi Yangu, kwa sababu, hadi sasa, watu bado hawajui lengo la mpango Wangu wa usimamizi, na hivyo leo bado husihi kimyakimya—na hili ni la faida gani?

Ninapoishi kati ya wanadamu, Nashikilia nafasi fulani katika mioyo ya watu; kwa kuwa Nimeonekana katika mwili, na watu wanaishi katika mwili wa zamani, wao kila mara hunishughulikia na mwili. Kwa sababu watu wana mwili tu, na hawana vijalizo vingine zaidi, wamenipa “yote waliyo nayo.” Lakini hawajui chochote, wao “hutoa ibada yao” tu mbele Yangu. Ninachovuna ni takataka isiyo na thamani—lakini watu hawafikiri hivyo. Ninapolinganisha “zawadi” walizotoa kwa vitu Vyangu, watu hutambua thamani Yangu mara moja, na wakati huo tu ndio wao huona kutopimika Kwangu. Sijivuni kwa sababu ya sifa zao, lakini Naendelea kuonekana kwa mwanadamu, ili watu wote waweze kunijua kwa ukamilifu. Nionyesha uzima Wangu kwao, wao hunitazama kwa macho yaliyokodoa, wakisimama mbele Yangu bila kujongea, kama nguzo ya chumvi. Na Ninapotazama kutokuwa kawaida kwao Mimi huwa na taabu kujizuia kucheka. Kwa sababu wananyosha mkono kuomba vitu kutoka Kwangu, Mimi huwapa vitu vilivyo mkononi Mwangu, nao huvikumbatia, wakitunza kama mtoto aliyezaliwa hivi sasa, ishara waifanyayo tu mara moja. Ninapobadilisha mazingira ambamo wanaishi, mara moja wao humtupa “mtoto mchanga” upande mmoja na kukimbia na vichwa vyao mikononi mwao. Machoni pa watu, Mimi ni msaada ambao upo bila kujali muda au mahali, ni kama kwamba Mimi ni mhadumu ambaye huja mara tu anapoitwa. Hivyo, watu daima “wamenitegemea,” kama kwamba Nina uwezo usio na kipimo wa kupambana na janga, na hivyo kila mara wameushika mkono Wangu, wakiniongoza kwenye safari kutoka upande mmoja hadi mwingine wa nchi, ili vitu vyote viweze kuona kwamba vina Mtawala, ili mtu yeyote asithubutu kuvidanganya. Nimebaini tangu zamani hila za watu za “mbweha kuchukua utukufu wa chui mwenye milia,” kwa maana wote “wananing’iniza mbwe zao,” wakitaka kufaidika kwa njia ya udanganyifu. Nimebaini tangu zamani mpango wao wenye kudhuru kwa siri, wenye nia mbaya, na ni vile tu Sitaki kuumiza uhusiano wetu. Sileti taabu bila sababu yoyote—hakuna thamani au umuhimu katika hilo. Mimi hufanya tu kazi ambayo ni lazima kwa sababu ya udhaifu wa watu; kama sivyo, Ningewageuza majivu na kutowaruhusu kuwapo tena. Lakini kazi Nifanyayo ina maana, na hivyo Simwadibu mwanadamu kwa urahisi. Ni kwa sababu hii ndiyo watu daima wameipa miili yao uhuru. Hawafuati mapenzi Yangu, lakini wamenirairai daima mbele ya kiti Changu cha hukumu. Watu ni wajasiri sana: Wakati vifaa vyote vya mateso vinapowatishia, hawawi na shaka hata kidogo. Kabla ya ukweli, wanasalia kutoweza kutoa ukweli wowote, na hawafanyi chochote ila kwa ukaidi hunipinga. Ninapowauliza kuleta yote yaliyo na uchafu, bado wananionyesha mikono miwili mitupu—wengine wangewezaje kukosa kutumia hili kama

“mfano”? Ni kwa kuwa imani ya watu ni kubwa mno ndio wao ni “wa kusifiwa.”

Nimeanza kazi Yangu kutoka upande mmoja hadi upande mwingine wa ulimwenguni; watu wa ulimwengu huamka ghafla, na kutembea wakizunguka kiini, ambayo ni kazi Yangu, na “Ninaposafiri” ndani yao, wote huepuka utumwa wa Shetani, na hawateswi katikati ya mateso ya Shetani. Kwa sababu ya majilio ya siku Yangu, watu hujaa furaha, huzuni ndani ya mioyo yao hutoweka, mawingu ya huzuni angani hugeuka kuwa oksijeni katika hewa na kuelea hapo, na wakati huu, Nafurahia furaha ya umoja na mwanadamu. Vitendo vya mwanadamu hunipa kitu cha kufurahia, na hivyo Sisikitishwi tena. Na, kuandamana na majilio ya siku Yangu, vitu vya dunia amabavyo vina nguvu, vitu vyote duniani huwa hai tena, na vinanikubali Mimi kama asili ya kuwepo kwao, kwa sababu Mimi Husababisha vitu vyote kuangaza na uzima, na hivyo, pia, Navisababisha kutoweka kimyakimya. Hivyo, vitu vyote husubiri amri kutoka kwa kinywa Changu, na hupendezwa na yale ambayo Ninafanya na kusema. Kati ya vitu vyote, Mimi ni Aliye Juu Zaidi—lakini Mimi pia Naishi miongoni mwa watu wote, na kutumia matendo ya watu kama maonyesho ya uumbaji Wangu wa mbingu na dunia. Wakati watu wanatoa sifa kubwa mbele Yangu, Mimi Husifiwa miongoni mwa vitu vyote, na hivyo maua duniani huwa mazuri zaidi chini ya jua kali, nyasi hustawi zaidi, na mawingu angani huonekana samawati zaidi. Kwa sababu ya sauti Yangu, watu hukimbia huku na kule; leo nyuso za watu katika Ufalme Wangu zimejaa furaha, na maisha yao yanakua. Ninafanya kazi miongoni mwa wateule Wangu wote, na Siruhusu kazi Yangu kutiwa doa na mawazo ya binadamu, kwani Mimi binafsi hutekeleza kazi Yangu Mwenyewe. Ninapofanya kazi, mbingu na dunia na kila kitu ndani yake hubadilika na kufanywa upya, na wakati Ninapokamilisha kazi Yangu, mwanadamu hufanywa upya kabisa, haishi tena katika huzuni kwa sababu ya kile Ninachouliza, kwani sauti za furaha zinaweza kusikika kutoka upande mmoja hadi upande mwingine wa dunia, na Mimi Huchukua nafasi hii kutoa miongoni mwa wanadamu baraka ambazo Mimi huwapa. Wakati Mimi ni Mfalme wa ufalme, watu huniogopa, lakini wakati Mimi ni Mfalme miongoni mwa wanadamu, na kuishi miongoni mwa wanadamu, watu hawafurahishwi nami, kwa maana dhana zao juu Yangu ni za kuhuzunisha sana, kiasi kuwa zimetiwa ndani sana kiasi cha kuwa ngumu kuondoa. Kwa sababu ya onyesho la mwanadamu, Nafanya Kazi Yangu, ambayo inafaa, na wakati Ninapoinuka juu mbinguni na kuachilia ghadhabu Yangu juu ya mwanadamu, maoni mbalimbali ya watu kunihusu mara moja hugeuka majivu. Nawaomba kunena dhana zao kadhaa zaidi Kwangu, lakini wamepigwa na bumbuwazi, kama kwamba hawana chochote, na kama kwamba wao ni wanyenyekevu. Kadri Ninavyoishi katika dhana za watu, ndivyo wanavyokuja kunipenda zaidi, na kadri Ninavyoishi nje ya dhana za watu, ndivyo wanavyozidi kunikwepa, na wana maoni zaidi kunihusu, kwani, tangu wakati Nilipoumba dunia mpaka leo, daima Nimeishi katika dhana za watu. Ninapokuja miongoni mwa wanadamu leo, Mimi huondoa dhana zote za watu, na

hivyo watu hukataa tu—lakini Nina mbinu zinazofaa za kushughulikia dhana zao. Watu wasiwe na wahaka au wasiwasi; Nitawaokoa wanadamu wote kwa mbinu Zangu Mwenyewe, na kuwafanya watu wote wanipende, na kuwaruhusu kufurahia baraka Zangu mbinguni.

Aprili 17, 1992

Sura ya 34

Wakati mmoja Nilimwalika mwanadamu kama mgeni nyumbani Kwangu, lakini alikimbia huku na huko kwa sababu ya miito Yangu—kama kwamba, badala ya kumwalika kama mgeni, Nilikuwa nimemleta kwenye eneo la kuuawa. Kwa hiyo, nyumba Yangu inaachwa tupu, kwa maana mwanadamu daima ameepukana na Mimi daima, na daima alijilinda dhidi Yangu. Hili liliniacha bila njia yoyote ya kutekeleza sehemu ya kazi Yangu, ambalo ni kusema, ni kama Nimeirudisha karamu Niliyomtayarishia, kwa maana mwanadamu hakuwa radhi kuifurahia karamu hii, na kwa hiyo Sikumlazimisha kufanya hivyo. Lakini mwanadamu ghafula hujikuta akizongwa na njaa, kwa hiyo anakuja kubisha mlangoni Mwangu akiomba msaada Wangu—na Nikimwona amepata mashaka kama hayo, Ningewezaje kukosa kumsaidia? Hivyo, kwa mara nyingine Namwandalia mwanadamu karamu, ili aweze kuifurahia, na wakati huo tu ndio anahisi jinsi Ninavyopendeka, na hivyo anakuja kunitegemea. Na kwa sababu ya mtazamo wangu kwake, anakuja kunipenda polepole “bila kusita,” na hashuku tena kwamba Nitamtuma katika “nchi ya uchomaji maiti,” kwani haya si mapenzi Yangu. Na kwa hiyo, ni baada ya kuona moyo Wangu tu ndio mwanadamu hunitegemea kweli, ambalo linaonyesha tu jinsi alivyo na “tahadhari”. Lakini Siwi macho kwa mwanadamu kwa sababu ya udanganyifu wake, lakini Husisimua mioyo ya watu kwa kumbatio Langu changamfu. Je, hili silo Nifanyalo sasa? Je, hili silo linalodhihirika ndani ya watu katika hatua ya sasa? Kwa nini wana uwezo wa kufanya mambo kama haya? Kwa nini wana hisia ya moyoni kama hiyo? Je, ni kwa sababu wananjua kwa kweli? Kwa sababu wana upendo usio na mipaka Kwangu kwa kweli? Simlazimishi mtu yeyote kunipenda, lakini Nampa tu uhuru wa kujifanyia uchaguzi wake mwenyewe; katika hili, Siingilii, wala kumsaidia kufanya uchaguzi kuhusu majaliwa yake. Watu waliweka uamuzi wao mbele Yangu, waliuleta mbele Yangu ili Niuchunguze, na wakati Nilipofungua mfuko ulio na “azimio la mwanadamu,” Niliona mambo yaliyovurugika ndani. Lakini mambo yaliyokuwa ndani yalikuwa “mengi,” na watu walinitazama kwa macho yaliyokodoa, wakiwa na hofu kubwa kwamba Ningeondoa azimio lao. Lakini kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu, Sikutoa hukumu mwanzoni kabisa, na badala yake Niliufunga mfuko na kuendelea kufanya kazi Niliyopaswa kufanya. Mwanadamu, hata hivyo, haingii katika mwongozo Wangu katika mwamko wa kazi Yangu, lakini anaendelea kujishughulisha na kama azimio lake limesifiwa na Mimi. Nimefanya kazi nyingi sana, Nimenena maneno mengi sana, lakini hadi sasa, mwanadamu

bado hawezi kuyaelewa mapenzi Yangu, na hivyo kila kitendo chake cha kushangaza kinaacha “kichwa Changu kikizunguka.” Kwa nini hawezi kuelewa mapenzi Yangu daima, na hufanya mambo kwa haraka kama appendavyo? Je, ubongo wake umepatwa na mshtuko? Inawezekana kuwa hafahamu maneno Nisemayo? Kwa nini yeye daima hutenda na macho yake yakiangalia mbele kabisa, lakini hawezi kuunda njia na kuonyesha mfano kwa watu wa baadaye? Je, kulikuwa na mtu yeyote wa kuonyesha mfano kabla ya Petro? Je, si chini ya mwongozo Wangu ndipo Petro akanusurika? Kwa nini watu wa leo hawawezi kufanya hili? Kwa nini, baada ya kuwa na mfano wa kufuata, bado hawawezi kuridhisha mapenzi Yangu? Hili linaonyesha kwamba bado mwanadamu hana imani Kwangu, ambalo ndilo limesababisha hali za leo zenye taabu.

Mimi hufurahia kuwatazama ndege wadogo wakipaa angani. Ingawa hawajaweka azimio lao mbele Yangu, na hawana maneno ya “kunipa” Mimi, wanapata raha katika ulimwengu ambao Nimewapa. Mwanadamu, hata hivyo, haliwezi hili, na uso wake umejaa huzuni—yawezekana kwamba Nina deni lake lisiloweza kulipwa? Kwa nini uso wake daima una michirizi ya machozi? Mimi hustaajabia mayungiyungi yanayochanuka vilimani. Maua na nyasi zinanyooka toka upande mmoja hadi upande mwingine wa miteremko, lakini mayungiyungi yanaongeza mng’aro kwa utukufu Wangu duniani kabla ya kufika kwa majira ya kuchipua—je, mwanadamu anaweza kutimiza kiasi hiki? Je, angeweza kunishuhudia duniani kabla ya kurudi Kwangu? Je, angeweza kujitolea kwa ajili ya jina Langu katika nchi ya joka kubwa jekundu? Ni kama kwamba matamko Yangu yamejaa matakwa kwa mwanadamu—ananichukia sana kwa sababu ya matakwa haya; kwa sababu mwili wake ni dhaifu sana, na hawezi kimsingi kufikia kile Ninachotaka, anaogopa maneno Yangu. Ninapofungua kinywa Changu, Nawaona watu duniani wakikimbia kila upande, kama kwamba wanajaribu kuitoroka njaa. Ninapofunika uso Wangu, wakati Ninapogeza mwili Wangu, watu ghafla huwa wanaingiwa na hofu, hawajui cha kufanya, kwani wanaogopa kuondoka Kwangu; katika dhana zao, siku Nitakayotoka ndiyo siku ambayo msiba utashuka kutoka mbinguni, siku Nitakayoondoka ndiyo siku ambayo adhabu yao itaanza. Lakini Ninachofanya ni kinyume kabisa na dhana za mwanadamu, Sijawahi kutenda kulingana na dhana za mwanadamu, Sijaruhusu kamwe dhana zake kuwa zenye kuchukua na Mimi. Wakati Ninapotenda ni wakati ambapo kwa usahihi mwanadamu anawekwa wazi. Kwa maneno mengine, vitendo Vyangu haviwezi kupimwa na dhana za binadamu. Tangu wakati wa uumbaji mpaka leo, hakuna mtu aliyewahi kugundua “bara mpya” katika mambo ambayo Ninafanya, hakuna mtu aliyewahi kuelewa sheria ambazo kwazo Ninatenda, hakuna mtu aliyewahi kufungua njia mpya. Hivyo, leo, watu bado hawawezi kuingia katika njia sahihi—ambayo ndiyo hasa wanayokosa, na wanayopaswa kuingia ndani yake. Tangu wakati wa uumbaji mpaka leo, Sijawahi kamwe kuanza shughuli kama hiyo hapo awali, Nimeongeza tu vipande

vipya kwa kazi Yangu katika siku za mwisho. Lakini hata chini ya hali kama hizo dhahiri, watu bado hawawezi kuelewa mapenzi Yangu—hiki sio kile ambacho wanakosa kabisa?

Baada ya kuingia katika kazi mpya, Nina matakwa mapya kwa mwanadamu. Kwa mwanadamu, ni kama kwamba matakwa ya zamani hayajakuwa na matokeo, ambayo ndiyo sababu anayasahau. Ni njia gani mpya ambayo kwayo Nafanya kazi? Ninataka nini kwa mwanadamu? Watu wenyewe wanaweza kupima kama yale waliyofanya katika siku za nyuma yalifuatana na mapenzi Yangu, ikiwa matendo yao yalikuwa ndani ya mipaka ya kile Nilichotaka. Hakuna haja ya Mimi kukagua kila kitu kimoja kimoja; wanaelewa kimo chao wenyewe, na kwa hiyo katika mawazo yao, wanaelewa wanaweza kutenda hadi kiasi gani, na hakuna haja ya Mimi kuwaambia waziwazi. Ninapozungumza, pengine, watu wengine watajikwaa; hivyo, Nimeepuka kusema sehemu hii ya maneno Yangu ili kuzuia watu kugeuka kuwa wadhaifu kutokana na hilo. Je, hili sio la manufaa makubwa zaidi kwa ufuatiliaji wa mwanadamu? Je, sio la manufaa makubwa zaidi kwa maendeleo ya mwanadamu? Nani hataki kusahau mambo yake ya zamani, na kujitahidi kuendelea mbele? Kwa sababu ya “kutofikiri” Kwangu, Sijui kama watu wanaelewa kuwa njia ambazo kwazo Nanena tayari zimeingia katika eneo jipya. Kwa kuongeza, kwa sababu kazi Yangu ni ya “shughuli nyingi,” sana, Sijakuwa na wakati wa kuuliza kama watu wanaelewa sauti ambayo kwayo Nanena. Hivyo, Nataka tu kwamba watu wanihurumie zaidi. Kwa sababu kazi yangu ni ya “shughuli nyingi,” sana, Siwezi binafsi kutembelea vituo vya kazi Yangu ili kuwaongoza watu, na kwa hiyo Nina “ufahamu mdogo” kuwahusu. Kwa jumla, chochote kingine, Nimeanza sasa kuongoza mwanadamu kuingia rasmi katika mwanzo mpya, na katika mbinu mpya. Katika matamko Yangu yote, watu wameona kwamba kuna kuchekesha, ucheshi, na sauti ya nguvu ya dhahaka hasa katika kile Ninachosema. Hivyo, maelewano kati ya mwanadamu na Mimi huvurugwa bila kujua, na kusababisha kifuniko kizito cha mawingu juu ya nyuso za watu. Mimi, hata hivyo, Sizuiliwi na hili, lakini Naendelea na kazi Yangu, kwani yote ambayo Nasema na kufanya ni sehemu ya lazima ya mpango Wangu, yote yanayonenwa kutoka kinywa Changu humsaidia mwanadamu, na hakuna chochote Nifanyacho ni cha upuuzi, lakini cha kuadilisha watu wote. Ni kwa sababu mwanadamu anapungukiwa ndio Naachilia huru na kuendelea kunena. Watu wengine, labda, wananisubiri bila tumaini Nitoe matakwa mapya kwao. Ikiwa ndivyo, basi Naridhisha mahitaji yao. Lakini kuna jambo moja ni lazima Niwakumbushe: Ninapozungumza, Natumai kuwa watu wanapata ufahamu zaidi, Natumai kuwa wanatambua zaidi, ili waweze kupata zaidi kutoka kwa maneno Yangu na hivyo kutimiza matakwa Yangu. Hapo awali, katika makanisa, lengo la watu lilikuwa ni kushughulikiwa na kuvunjwa. Kula na kunywa Maneno yangu kulikuwa juu ya msingi wa kuelewa malengo yao na chanzo—lakini leo si kama siku za nyuma, watu hawawezi kabisa kuelewa chanzo cha matamko Yangu, na hivyo hawana nafasi ya kushughulikiwa na

kuvunjwa na Mimi, kwa sababu wao wametumia kila kitu walicho nacho kula na kunywa maneno Yangu. Lakini hata katika hali hizi, bado hawawezi kuridhisha matakwa yangu, na hivyo Nafanya madai mapya kwao: Nawataka waingie katika majaribio pamoja nami, kwamba waingie katika kuadibu. Lakini hebu Niwakumbushe jambo moja: Huku si kumwua mwanadamu, lakini kinachohitajika na kazi Yangu, kwa kuwa, katika hatua ya sasa, maneno Yangu hayaeleweki kabisa na mwanadamu, na mwanadamu hawezi kushirikiana na Mimi—hakuna cha kufanya! Naweza tu kumfanya mwanadamu aingie katika utaratibu mpya pamoja nami. Kuna nini kingine cha kufanya? Kwa sababu ya kasoro za mwanadamu, Mimi pia lazima Niingie katika mkondo ambao mwanadamu huingia—je, si Mimi ambaye atawafanya watu wawe kamili? Je, si Mimi Niliyeonyesha mpango huu? Ingawa matakwa yale mengine si magumu, si ya pili kwa ya kwanza. Kazi Yangu kati ya kundi la watu wa siku za mwisho ni shughuli iliyo ya pekee, na hivyo, ili utukufu Wangu uweze kujaza ulimwengu, watu wote lazima wapitie taabu ya mwisho kwa ajili Yangu Mimi. Je, unaelewa mapenzi Yangu? Haya ndiyo matakwa ya mwisho ambayo Nataka kutoka kwa mwanadamu, ambalo ni kusema, Natumai kwamba watu wote wanaweza kutoa ushuhuda wenye nguvu, unaovuma Kwangu mbele ya joka kubwa jekundu, kwamba waweze kujitolea wenyewe Kwangu kwa mara ya mwisho, na kutimiza matakwa Yangu kwa mara nyingine ya mwisho. Je, nyinyi mnaweza kufanya hili kweli? Nyinyi hamkuweza kuuridhisha moyo Wangu katika siku zilizopita—je, mnaweza kuvunja mpangilio huu katika mara ya mwisho? Nawapata watu fursa ya kutafakari, Nawaacha watafakari kwa makini kabla ya kunipa jibu hatimaye—je, ni kosa kufanya hili? Nasubiri jibu la mwanadamu, Nangoja “barua yake ya kujibu”—je, nyinyi mna imani ya kutimiza matakwa Yangu?

Aprili 20, 1992

Sura ya 35

Nimeanza kutenda kazi Yangu kati ya wanadamu, kuwakubalia kuishi mkondo mmoja Nami. Nitakamilisha kazi Yangu nikiwa kati yao, maana wao ni vyombo Ninavyosimamia katika mpango Wangu wote wa usimamizi—na ni mapenzi Langu ili waweze kuwa watawala wa vitu vyote. Hivyo basi Naendelea kutembea kati ya wanadamu. Kadri wanadamu pamoja Nami tuingiavyo katika enzi ya sasa, Najihisi huru kabisa, kwa sababu, hatua Yangu ni ya haraka. Wanadamu hawa wanawezaje kudumisha mwendo huu? Nimefanya kazi nyingi kwa watu wasiojali na walio butu, lakini hawajafaidi chochote kwa kuwa hawanijali wala kunipenda Mimi. Nimeishi kati ya watu wote na kuwatazama waendapo juu na chini ya ardhi. Wale wote wanaoainishwa kama “wanadamu” wananipinga Mimi, kana kwamba “kunipinga Mimi” kulikuwa katika maelezo ya kazi yao. Inaonekana kwamba kama hawangeitekeleza hii kazi, basi wangekuwa kama yatima mzururaji, asiypangwa na mtu yeyote. Hata hivyo, Mimi

Siwahukumu watu kwa udhalimu kulingana na matendo na tabia zao. Bali, Mimi husaidia na kuwaruzuku kwa mujibu wa kimo chao. Kwa kuwa wanadamu ndio wahusika wakuu wa mpango Wangu wote wa usimamizi, Ntoa ushauri zaidi kwa walio katika hii nafasi ya “binadamu” ili waweze kuigiza kwa moyo wote na kwa uwezo wao wote, ili igizo hili Ninaloliongoza liweze kufanikiwa kikamilifu. Hili ndilo ombi Langu kwa wanadamu. Je, yawezekana kuwa bila ombi hili, hawataweza kutenda wajibu wao kadri ya uwezo wao? Naweza kutimiza kile watu wanachohitaji Kwangu, lakini wao hawawezi kutimiza Ninachohitaji kwao? Inaweza kusemwa kwamba situmii nguvu zangu kumtesa mwanadamu. Badala yake, hili ni ombi Langu la mwisho, ambalo Nawasihi kwa ukunjufu na uaminifu wote. Hawawezi kwa kweli kufanya Ninachowauliza? Nimekuwa nikiwapa watu kwa miaka mingi, lakini Sijapokea chochote kutoka kwao. Ni nani amewahi kunipa Mimi chochote? Je, damu, jasho, na machozi Yangu ni kama tu mawingu milimani? Nimewapa watu “chanjo” mara nyingi, na kuwaambia kwamba mahitaji Yangu kwao hayakuwa ya kushurutisha. Kwa nini, basi, watu huniepuka Mimi daima? Je, ni kwa sababu Nitawachukulia kama vifaranga wadogo, kuuawa punde washikwapo? Je, Mimi ni katili na asiye na huruma hivyo? Wanadamu daima hunipima kwa mizani ya fikira zao. Je, Mimi nipo katika fikira zao, jinsi Nilivyo mbinguni? Sichukulii fikira za watu kuwa vyombo vya furaha Yangu. Bali, Naiona mioyo yao kama vitu vya kuthaminiwa. Hata hivyo, Nahisi kuchoshwa kabisa na dhamiri zao, kwa kuwa kulingana na wao, Mimi Mwenyewe sina dhamiri. Hivyo basi Nimefafanua kauli za ziada juu ya mada hiyo. Hivyo, Nina maoni kadhaa zaidi kuhusu dhamira zao. Hata hivyo, Nakataa kukosoa dhamiri zao moja kwa moja; badala yake, Naendelea kuwaelekeza kwa uvumilivu na utaratibu. Hata hivyo, wanadamu ni dhaifu, na hawawezi kuifanya kazi yoyote.

Leo, Nimechukua hatua rasmi kuingia katika eneo la kuadibu kusio na mipaka, na Ninaifurahia pamoja na wanadamu. Pia Nawaongoza kwa mkono, nao wana nidhamu njema chini ya uongozi Wangu; hakuna anayethubutu kunipinga Mimi. Wote wapo chini ya uongozi Wangu, wakiteleza wajibu Niliowapa, kwa kuwa hili lipo katika “maelezo ya kazi” zao. Kati ya mambo yote yaliyo mbinguni na chini ya mbingu ni nani huthubutu kutotii mipango Yangu? Ni nani asiye katika mfumbato Wangu? Ni nani asiyetamka sifa na fadhili kwa maneno Yangu na kazi Zangu? Wanadamu huajabia matendo Yangu, hivyo basi wao hujitoa kwa mkondo wa kazi Yangu kwa ajili ya kila hatua Yangu ndogo. Ni nani awezaye kuacha? Ni nani anayeweza kuondoka kutoka kwa kazi Niliyoipanga? Kwa ajili ya amri Yangu ya utawala, wanadamu hawana budi ila kusalia; bila hiyo, wote wangepenyeza kimya kimya kutoka “mstari wa mbele” na kuwa “watoro.” Nani asiye na hofu ya kifo? Je, inawezekana watu kuhatarisha maisha yao? Simlazimishi yeyote, kwa sababu Nilipata ufahamu wa asili ya wanadamu hapo kale. Kwa hivyo, Nimekuwa kila mara Nikifanya miradi ambayo watu hawajawahi kufanya hapo awali. Kwa kuwa hakuna mtu ambaye

angeifanya kazi Yangu, Nimeingia vitani binafsi kukumbana na mapambano ya kufa na kupona dhidi ya Shetani. Siku hizi, Shetani amekithiri kupita kiasi. Kwa nini Nisichukue fursa hii kuringia kiini cha kazi Yangu ili kufichua nguvu Zangu? Kama Nilivyosema hapo awali, Natumia ujanja wa Shetani kama foili^[a]; je, hii sio fursa mwafaka? Sasa tu ndio Naonyesha tabasamu ya kufurahishwa, maana Nimetimiza lengo Langu. Sitakimbia huku na huku tena na kuomba ‘msaada’ wa wanadamu. Nimeacha kutangatanga huku na huko, na Siishi tena maisha ya mzururaji. Tangu sasa kuendelea, Nitaishi kwa amani. Wanadamu pia watakuwa salama salmini, kwa maana siku Yangu imewadia. Hapa duniani Nimeishi maisha ya shughuli nyingi mno ya mwandamu, maisha ambamo matukio mengi ya udhalimu yanaonekana yamefanyika. Kwa macho ya wanadamu, Nimeshiriki raha na masikitiko yao, na vilevile shari zao. Kama wanadamu, Mimi, pia, Nimeishi duniani na chini ya mbingu. Hivyo basi wameniona Mimi daima kama kiumbe kilichoumbwa. Kwa kuwa wanadamu hawajaniona Mimi mbinguni, hawajatumia juhudi nyingi Kwangu. Hata hivyo, hali ilivyo leo, watu hawana budi ila kukubali kuwa Mimi ni Bwana wa majaliwa yao na mnenaji anenaye kutoka mawinguni. Hivyo basi wanadamu wamegusisha vichwa vyao ardhini wakiabudu mbele Yangu. Je, hii sio ithibati ya marejeo Yangu ya ushindi? Je, hili silo onyesho la ushindi Wangu dhidi ya majeshi yote ya uhasama? Watu wote wamekuwa na jakamoyo kwamba dunia inakaribia mwisho, na kwamba binadamu utapitia utakaso mkuu. Hata hivyo, hawawezi kwa ukweli kutimiza kwa kufahamu kile Ninachouliza, kwa hiyo hawana budi ila kulia chini ya kuadibu Kwangu. Nini kinachoweza kufanyika? Ni nani aliyewaambia hawa wanadamu kutotii? Ni nani aliyewaambia kuingia katika enzi ya mwisho? Kwa nini walizaliwa kwa ulimwengu wa wanadamu katika siku hizi za mwisho? Kila kimoja kimepangwa na Mimi binafsi. Ni nani anayeweza kutamka malamiko?

Tangu uumbaji wa ulimwengu, Nimetembea kati ya wanadamu, Nikiishi nao katika kuishi kwao duniani. Katika vizazi vilivyotangulia, hata hivyo, hakuna mtu hata mmoja aliyechaguliwa na Mimi; wote walikataliwa na kimya cha barua Yangu. Hii ni kwa sababu watu hao wa kale hawakunitumikia Mimi pekee; kwa hivyo Mimi, kwa malipo Sikuwapenda kipekee. Wao walichukua “zawadi” za Shetani na kisha wakageuka na kunitolea Mimi; Je, hii si kashfa dhidi Yangu? Na walipotoa sadaka zao Sikufichua ghadhabu Yangu; Mimi nilibadili mpango wao kwa matumizi Yangu mwenyewe kwa kuongezea “zawadi” hizi kwa vifaa Ninavyotumia katika usimamizi Wangu. Baadaye, mara tu vilipokuwa vimesindikwa na mtambo, Ningechema taka zilizo ndani. Katika kizazi hiki, wanadamu hakijanitolea Mimi “vipawa” vingi, Siwakaripii kwa hayo. Watu hawa wamekuwa daima masikini na wenye mkono mtupu; hivyo, kwa kutazama uhalisi wa hali yao, Sijawahi kuwaitisha kisichowezezekana baada ya Mimi kuja katika ulimwengu wa wanadamu. Bali, baada ya kuwapa “vifaa,” Nimetafuta tu “bidhaa iliyokamilishwa” Ninayotaka, maana hili ndilo jambo pekee la kuweza kutimizwa na wanadamu. Nimeishi miaka

mingi kwenye taabu, Nikijifunza maana ya kuishi kama mwanadamu, kabla ya kutoa ombi la kufaa. Lau Singekuwa na uzoefu wa maisha ya mwanadamu, Ningeelwaje maswala wanayoyaona magumu kujadili? Hata hivyo, wanadamu hawayaoni hivi; wao husema tu Mimi ni Mungu mwenye nguvu, Mungu Mwenyewe wa ajabu. Je, hii siyo hasa dhana ambayo wanadamu wote wamekuwa nayo kote katika historia na hata mpaka leo? Nilisema kuwa ardhini hakuna yeyote anayeweza kunijua Mimi kweli asilimia mia moja. Usemi huu una maana yake; hii sio porojo tu. Nina uzoefu na Nimeona hili Mimi Mwenyewe, kwa hivyo Nina ufahamu wa utondoti. Iwapo Singekuja chini kwa ulimwengu wa wanadamu, ni nani angekuwa na nafasi ya kunijua Mimi? Ni nani angeyasikiliza maneno Yangu binafsi? Ni nani angeona umbo Langu kati yao? Tangu nyakati za zamani Nilikuwa daima Nimefichwa mawinguni. Nilitabiri hapo mapema kwamba Ningeshuka chini kwa ulimwengu wa wanadamu katika siku za mwisho kuwa mfano wao mzuri. Ndio maana siku hizi watu wana bahati kupanua peo zao. Je, hii si fadhili Niliyowakidhi nayo? Je, yawezekana kuwa hawataelewa neema Yangu kabisa? Mbona wanadamu ni wasiojali hisia za wengine na ni butu sana? Baada ya kuja umbali huu, mbona bado hawajaamka? Nimekuwapo humu ulimwenguni kwa miaka mingi lakini nani anijuaye? Si ajabu Nawaadibu watu. Inaonekana kwamba wao ndio vyombo vya kuweka mamlaka Yangu katika matumizi; inaonekana kwamba wao ni risasi kwenye bunduki Yangu ambazo, Nikishalipua, zote zitapotea. Hili ndilo wazo lao. Nimewaheshimu wanadamu daima; Sijawahi kuwanyonya kwa udhalimu au kuwafanyia biashara kama watumwa. Hii ni kwa sababu Siwezi kuwaacha, wala wao hawawezi kuniwacha Mimi. Hivyo basi, mshikamano wa kufa kupa umeundwa kati Yetu. Daima Nimempenda mwanadamu. Ijapokuwa mwanadamu hajawahi kuwa mwenye upendo Kwangu, daima, ndio maana Naendelea kutumia juhudi kwao. Nawapenda watu kama hazina Yangu mwenyewe, maana wao ndio “rasilimali” ya usimamizi Wangu duniani; hivyo basi Sitawaangamiza kamwe. Mapenzi Yangu kwa wanadamu hayatabadilika. Je, wanaweza kusadiki kwa kweli katika kiapo Changu? Watawezaje kuniridhisha? Huu ndio wajibu wa wanadamu wote; hili ndilo “zoezi la nyumbani” Nililowaachia. Ni tumaini Langu kwamba wote watafanya bidii kulikamilisha.

Aprili 23, 1992

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Sura ya 36

Kila kitu kinapangwa kwa mkono Wangu. Nani anathubutu kufanya anavyopenda? Nani anayeweza kukibadilisha kwa urahisi? Watu huelea hewani, wakienda mbele kama vumbi

linavyokwenda, nyuso zao zimejaa uchafu, kuwafanya wasivutie kutoka utosini hadi wayoni. Mimi huangalia kutoka miongoni mwa mawingu na moyo mzito: Kwa nini mwanadamu, ambaye wakati mmoja alijaa uhai, amegeuka kuwa namna hii? Na kwa nini hajui jambo hili, na kutohisi jambo hili? Kwa nini “anajiachilia” na kujiruhusu kufunikwa kwa uchafu? Huo ndio ukosefu wake wa upendo na heshima kwake. Kwa nini mwanadamu daima huepuka Ninachouliza? Je, Mimi ni mkatili na mnyama kwake kweli? Je, Mimi kweli ni dhalimu na Asiye na huruma? Hivyo kwa nini watu daima hunitazama kwa macho makali? Kwa nini daima wao hunichukia? Je, Nimewaleta mpaka ukingoni? Mwanadamu hajawahi kugundua chochote katika kuadibu Kwangu, kwani hafanyi chochote ila kushika nira inayozunguka shingo kwa mikono miwili, macho yake mawili yakiwa yamekodolewa Kwangu, kana kwamba anamwangalia adui kwa makini—na wakati huu tu ndio Nahisi vile amedhoofishwa. Ni kwa sababu ya hili ndio Nasema hakuna yeyote aliyewahi kusimama imara katikati ya majaribio. Je, kimo cha mwanadamu hakiko hivyo kabisa? Je, Nahitaji kumwambia tarakimu za “vipimo” vyake? “Urefu” wa mwanadamu sio mkubwa zaidi kuliko ule wa mnyoo mdogo anayejinyonganyonga juu ya ardhi, na “kifua” chake ni upana sawa tu na wa nyoka. Katika hili, mimi Simdunishi mwanadamu—je, hizi sizo tarakimu kamili za kimo chake? Je, Nimemshusha daraja mwanadamu? Mwanadamu ni kama mtoto anayechezacheza. Kuna hata nyakati ambapo anacheza na wanyama, lakini bado anabaki na furaha; na yeye ni kama paka, akiishi maisha bila kujali au wasiwasi. Labda ni kwa sababu ya mwelekeo wa Roho, au jukumu la Mungu mbinguni, ndio Najisikia mchovu sana kuhusu maisha ya ubadhirifu ya watu duniani. Kwa sababu ya maisha ya mwanadamu—ambayo ni kama ya kupe—“Shauku” Yangu katika maneno “maisha ya binadamu” imeongezeka kwa kiasi fulani, na hivyo Nimekuwa “mwingi wa heshima” zaidi kidogo kwa maisha ya binadamu. Kwa maana inaonekana kwamba mwanadamu pekee ndiye anaweza kuunda maisha ambayo yana maana, wakati ambapo Siwezi kufanya hivyo. Kwa hivyo Naweza tu kwenda kwenye “milima,” kwa maana Siwezi kupitia na kuchunguza shida miongoni mwa wanadamu. Lakini mwanadamu ananishurutisha kwa haraka—Sina budi! Ninaweza tu kutii mipango ya mwanadamu, kufupisha uzoefu pamoja naye na kupitia maisha ya binadamu pamoja naye. Mbinguni, wakati mmoja Nilitalii jiji lote, na chini ya mbinguni, wakati mmoja Nilitalii nchi zote. Lakini hakuna mtu aliyewahi kunitambua, walisikia tu sauti ya mwendo Wangu Nilipokuwa Natembea kote. Machoni pa watu, Mimi huja na kwenda Nisionekane tena. Ni kama kwamba Nimekuwa sanamu isiyoonekana ndani ya mioyo yao, lakini watu hawaamini hivyo. Yawezekana kuwa yote haya si ukweli uliokiriwa na kinywa cha mwanadamu? Wakati huu, ni nani asiyekubali kwamba anapaswa kuadibiwa? Je, watu bado wangejamini kabla ya ushahidi thabiti?

Nafanya mapatano ya biashara miongoni mwa wanadamu, Naufuta uchafu wake wote na

udhalimu wake, na hivyo “Namtengeneza” ili apate kuupendeza moyo Wangu. Lakini ushirikiano wa mwanadamu ni wa lazima kwa hatua hii ya kazi, kwa sababu yeye daima huchupa na kuruka kote kama samaki ambaye amevuliwa hivi sasa. Kwa hiyo ili kuzuia ajali zozote, Niliwaua samaki wote waliokuwa wamevuliwa, baada ya hilo samaki hao wakawa watiifu, na hawakuwa na malalamiko hata kidogo. Ninapomhitaji mwanadamu, daima huwa amejificha. Ni kana kwamba hajawahi kamwe kuona maonyesho ya kustaajabisha, kana kwamba alizaliwa mashambani na hajui chochote kuhusu mambo ya mjini. Naongeza hekima yangu kwa sehemu za mwanadamu ambazo zina upungufu, na kumfanya anijue Mimi; kwa sababu mwanadamu ni maskini sana, Mimi binafsi huja miongoni mwa wanadamu na kuwapa “njia ya kupata utajiri,” na kumfanya afumbue macho yake. Katika hili, je, Simwokoi? Je, hii si huruma Yangu kwa mwanadamu? Je, upendo ni kutoa bila masharti? Je, basi chuki ni kuadibu? Nimemwelezea mwanadamu kwa taswira tofauti, lakini analichukulia hili kama maneno na kanuni tu. Ni kama maneno Yangu ni bidhaa za daraja la pili, ambazo huuzwa kama vitu visivyo na thamani tena katika mikono ya mwanadamu. Hivyo, wakati Ninapowaambia watu kuwa dhoruba kubwa inakuja kumeza kijiji cha mlima, hakuna mtu anayefikiri chochote juu yake, ni wachache tu wanaohamisha nyumba zao, mioyo yao ikiwa na shaka. Wengine hawahami, kama kwamba hawajali, kama kwamba Mimi ni mbayuwayu kutoka angani—hawaelewi chochote kati ya yale Nisemayo. Ni wakati ambapo tu milima hupinduliwa na dunia kutenganishwa mbalimbali ndio watu hufikiria kuhusu maneno Yangu, wakati huo tu ndio wao huamshwa kutoka kwa ndoto zao, lakini wakati umefika tayari, wamemezwa katika mafuriko makuu, maiti yao yaelea juu ya maji. Kuona taabu ulimwenguni, Nashusha pumzi kwa msiba wa mwanadamu. Nilitumia muda mwingi, na kulipa gharama kubwa, kwa ajili ya majaliwa ya mwanadamu. Katika mawazo ya watu, Sina michirizi ya machozi—lakini Mimi, “dubwasha” huyu asiye na michirizi ya machozi, Nimelia machozi mengi kwa ajili ya mwanadamu. Mwanadamu, hata hivyo, hajui lolote kuhusu hili, anacheza tu na vidude vya kuchezea watoto mikononi mwake duniani, kama kwamba Siishi. Hivyo, katika hali za leo, watu hubakia sugu na wajinga, bado “wameganda” katika sehemu za nyumba zilizo chini ya ardhi, kama kwamba bado wanalala pangoni. Kuona vitendo vya mwanadamu, chaguo Langu la pekee ni kuondoka ...

Machoni pa watu, Nimefanya mengi ambayo ni mazuri kwa mwanadamu, na hivyo wananitazama kama mfano mwema wa enzi ya sasa. Lakini hawajawahi kamwe kunifikiria kama Mtawala wa majaliwa ya mwanadamu na Muumba wa vitu vyote. Ni kama kwamba hawanielewi. Ingawa wakati fulani watu walitangaza “Ufahamu udumu,” hakuna yeyote ambaye ametumia muda mwingi kuchambua neno ‘ufahamu,’ kuonyesha kwamba watu hawana hamu ya kunipenda. Katika nyakati za leo, watu hawajawahi kunithamini, Sina nafasi ndani ya mioyo yao. Je, wataweza kuonyesha upendo wa kweli Kwangu katika siku zijazo za mateso? Haki ya

mwanadamu inabaki kitu bila umbo, kitu ambacho hakiwezi kuonekana wala kuguswa. Nitakacho ni moyo wa mwanadamu, kwa kuwa katika mwili wa mwanadamu moyo ndio wa thamani sana. Je, matendo Yangu hayafai kulipwa kwa moyo wa mwanadamu? Kwa nini watu hawanipi mioyo yao? Kwa nini daima huikumbatia kwa vifua vyao wenyewe, wasitake kuiwacha? Je, moyo wa mwanadamu unaweza kuhakikisha amani na furaha katika maisha yote ya watu? Kwa nini, wakati Ninapotaka vitu kutoka kwa watu, wao daima kiasi kidogo cha vumbi kutoka ardhini na kulirusha Kwangu? Je, huu ni mpango wa hila wa mwanadamu? Ni kama kwamba anajaribu kumdanganya mpita njia ambaye hana mahali popote pa kwenda, akimshawishi arudi nyumbani kwake, ambako anageuka kuwa mbaya na kumuua. Watu wametaka pia kufanya mambo kama hayo Kwangu. Ni kama kwamba wao ni chakari ambaye atamuua mtu bila kujali, kama kwamba wao ni mfalme wa pepo, ambaye asili yake ya pili ni kuua watu. Lakini sasa watu huja mbele Yangu, bado wakitaka kutumia njia hizo—lakini wana mipango yao, na Nina mipango Yangu ya kupinga. Ingawa watu hawanipendi, Ningewezaje kukosa kuifanya mipango yangu ya kupinga wazi kwa mwanadamu wakati huu? Nina ujuzi usio na kikomo, usiopimika katika kumshughulikia mwanadamu; kila sehemu yake Hushughulikiwa binafsi na Mimi, na kutengenezwa binafsi na Mimi. Hatimaye, Nitamfanya mwanadamu avumilie maumivu ya kujitenga na kile anachopenda, na kumfanya atii mipango Yangu, na wakati huo, watu watalalamikia nini? Je, yote Nifanyayo si kwa ajili ya mwanadamu? Katika nyakati zilizopita, Sikuwahi kumwambia mwanadamu hatua za kazi Yangu—lakini leo, katika wakati usiofanana na uliopita, kwa sababu maudhui ya kazi Yangu ni tofauti, Nimewaambia watu juu ya kazi Yangu mapema ili kuwazuia kuanguka chini kutokana na hili. Je, hii siyo chanjo ambayo Nimeidunga sindano ndani ya mwanadamu? Kwa sababu yoyote ile, watu hawajawahi kuzingatia maneno Yangu kwa makini; ni kama kwamba kuna njaa ndani ya matumbo yao na si wagumu kupendeza kuhusu kile wanachokula, ambacho kimefanya matumbo yao kuwa dhaifu. Lakini watu huchukua “gimba yao bora” kuwa rasilimali na hawatambui maonyo ya “daktari.” Kwa kuona ukaidi wao, Najikuta Nikisikitika kwa ajili ya mwanadamu. Kwa sababu watu si wakovu, na bado hawana uzoefu wa maisha ya binadamu, hawana hofu; mioyoni mwao, maneno “maisha ya binadamu” hayapo, hawayajali, na huchoka tu na maneno Yangu, kama kwamba Nimekuwa mwanamke mzee mwenye kuparaganyaparaganya. Kwa jumla, kwa vyovyote vile, Natumai kwamba watu wanaweza kuelewa moyo Wangu, kwa maana Mimi Sina hamu ya kumtuma mwanadamu katika nchi ya kifo. Natumai kwamba mwanadamu anaweza kuelewa ni nini hisia Zangu kwa wakati huu, na kujali mzigo Ninaobeba hasa wakati huu.

Aprili 26, 1992

Sura ya 37

Kotekote katika enzi, kazi yote Niliyoifanya—kila hatua ya kazi hiyo—imekuwa na mbinu Zangu zinazofaa za kazi. Ni kwa sababu ya hili ndio watu Wangu wapendwa wamekuwa watakatifu zaidi na zaidi, na wa kufaa zaidi na zaidi kwa matumizi Yangu. Kwa sababu hiyo hiyo, hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kwamba kadri mbinu Zangu za kazi zinavyoongezeka, idadi ya watu inapungua, ambalo husababisha watu kuzama katika kutafakari. Bila shaka, Kazi Yangu leo sio tofauti na watu wengi wamejikuta tena katika kutafakari, kwa hiyo kwa sababu ya mabadiliko ya mbinu Zangu, kuna sehemu ya watu ambao watajiondoa. Inaweza kuelezwa kwa njia hii: Hili lilikuwa limeamuliwa na Mimi kabla, lakini halikufanywa na Mimi. Kutoka wakati wa uumbaji hadi sasa, watu wengi sana wameanguka na wengi sana wamepoteza njia yao kwa sababu ya mbinu za kazi Yangu, lakini Sijali kuhusu vile watu walivyo, kama wanahisi Sina moyo wa kupenda au kama wanahisi Mimi ni mkatili mno, na haijalishi kama ufahamu wa watu ni sahihi au la, Naepuka kutoa maelezo. Hebu kwanza tuwe na ushirika juu ya suala kuu la mjadala huu ili kila mtu awe na ufahamu kamili, na ili aweze kuepuka mateso yoyote yasiyoelezeka. Sitawalazimisha watu kuteseka kimya kama bubu. Badala yake, Nitaelezea kila kitu wazi ili watu wasilalamike Kwangu, na siku moja watu wote watatamka sifa ya kweli katikati ya kuadibu. Je, Hilo litafaulu? Je, Hilo linakidhi mahitaji ya watu?

Katika utangulizi wa enzi ya kuadibu, Nitawaambia watu maana ya jumla ya “enzi” hiyo kwanza ili wasinikosee. Yaani, Nitafanya utaratibu wa kazi Yangu, ambao hautabadilishwa na yeyote, na Sitamsamehe kabisa mtu yeyote anayeubadilisha bali Nitamshutumu. Je, mtakumbuka hilo? Hilo lote ni onyo la kutangulia. Katika mbinu mpya watu wote lazima kwanza waelewe kwamba jambo la kwanza na la awali kutimiza ni kuwa na ufahamu wa hali zao wenyewe. Kabla ya kupata ufahamu fulani wa mtu mwenyewe, hakuna mtu atakayeruhusiwa kuzungumza ovyo ovyo kanisani, na hakika Nitawaadibu wale wanaokiuka hili. Kuanzia siku hii kwenda mbele, mitume wote wataorodheshwa katika makanisa na kuzuiwa kwenda huku na kule; hilo lilileta matokeo kidogo. Wote walionekana kutimiza wajibu wao lakini walikuwa kweli wakinidanganya. Bila kujali vile wakati uliopita ulikuwa, leo yote yanapita na hayapaswi kutajwa tena. Tangu sasa na kuendelea, neno “mtume” litafutwa na kamwe halitatumikiwa tena, kwa hiyo watu wote waweze kushuka kutoka kwa nafasi zao na wajijue. Hili bila shaka ni kwa ajili ya wokovu wao. “Cheo” si taji, ni neno la kutaja mtu tu. Je, mnaelewa maana Yangu? Wale ambao wanaongoza makanisa bado wataishi maisha ya kanisa ndani ya makanisa yao wenyewe, na bila shaka, hii si kanuni ngumu. Ikilazimu wanaweza kutembelea makanisa kwa uratibu wa mitume wengine wa zamani. Jambo muhimu zaidi ni kwamba ushirika wa makanisa lazima uongezwe ila kama hakuna washirika wa makanisa wanaoishi kweli maisha ya kanisa. Hata hivyo, lazima Nisisitize kwamba lazima nyote muungane ili mjijue na kuasi lile joka kubwa

jekundu. Hii ni nia Yangu. Kiasi ambacho watu wanazungumza si muhimu, badala yake ni muhimu sana kwamba watu Wangu wote waweze kuja pamoja kama kitu kimoja, ambayo ni njia pekee ya kushuhudia kweli. Zamani, kila mtu alisema alijielewa, lakini Nimetamka maneno yasiyohesabika, na ni kiasi gani ambacho mmejielewa? Kadri cheo cha mtu kilivyo juu zaidi, ndivyo inavyokuwa vigumu zaidi yeye kujiweka kando. Zaidi ya hayo, kadri matumaini ya mtu yalivyo makuu, ndivyo atakavyoteseka wakati wa kuadibu. Huu ni wokovu Wangu wa wanadamu—je, mnaelewa? Msichukulie hili juujuu tu. Kufanya hivyo ni duni sana na hakuna thamani; Je, mnaelewa maana ya msingi? Kama watu katika kanisa wanaweza kweli kujifahamu, hili linadhihirisha kwamba mtu wa aina hii ananipenda Mimi kweli. Ni kama msemu, “Msipomega mkate na watu huwezi kuelewa shida zao.” Mnayaelewaje maneno haya? Mwishowe, Nitawafanya watu wote wapate kujifahamu wakati wa kuadibu, na kufanya waimbe na kucheka wakati wa kuadibu. Je, kweli utakuwa na imani ya kuniridhisha? Kwa hiyo unapaswa kufanya nini katika utendaji wako? Kuanzia sasa kuendelea, shughuli za kila kanisa zitashughulikiwa na watu wanaofaa katika kanisa hilo, na mitume wataishi tu maisha ya kanisa. Hiyo inaitwa “kuyapitia maisha.” Je, mnaelewa?

Kabla ya kuadibu kuwajia wanadamu rasmi, Nitafanya kwanza “kazi ya salamu” kwa watu ili mwisho wao wote waniridhishe. Hata kwa wale ambao wataondoka, lazima wateseke na kumaliza ushuhuda wao kabla ya kuondoka, la sivyo Sitawasamehe. Hii inaonyesha hali Yangu ya kutovumilia makosa ya watu, na hali Yangu ya kufanikisha kile Ninachosema. Kwa hiyo, inatimiza maneno kutoka kinywa Changu “Namaanisha kile Ninachosema, na kile Ninachomaanisha kitafanikishwa, na kile Ninachofanikisha kitadumu milele.” Maneno yanapotoka kinywani Mwangu, ndivyo Roho Wangu pia anaanza kazi Yake. Ni nani angethubutu kwa hiari kucheza na “mwanaserere” ulio mikononi mwake? Watu lazima wakubali kuadibu Kwangu kwa staha na kwa utiifu, na ni nani anayeweza kukuepuka? Je, Kunaweza kuwa na njia nyingine ila Mimi? Leo Nimekuruhusu uwe juu ya dunia, na ufurahi. Kesho Nitakuruhusu kwenda mbinguni na utasifu. Siku baada ya hiyo, Nitakuweka chini ya ardhi ambapo utaadibiwa. Je, hayo yote siyo matakwa ya kazi Yangu? Ni nani asiyepatwa na taabu, na ni nani asiyepokea baraka kwa ajili ya matakwa Yangu? Je, mnaweza kuwa tofauti? Kama watu Wangu duniani, mnapaswa kufanya nini kwa ajili ya matakwa Yangu, kwa ajili ya mapenzi Yangu? Je, inawezekana kwamba mnalitukuza jina Langu takatifu kwa vinywa vyenu lakini ndani ya mioyo yenu mnanichukia sana? Kunifanyia kazi, kuridhisha moyo Wangu, pamoja na kujielewa wenyewe na kuasi joka kubwa jekundu si kazi rahisi na lazima mlipe gharama ili kufanya hivyo. Ninaposema “gharama” mnalielewaje hilo? Sitalijadili hivi sasa kwa kuwa Siwapi watu majibu ya moja kwa moja. Badala yake, Nawaruhusu wote kulifikiria wenyewe, na baadaye, watumie vitendo na tabia zao kujibu maswali Yangu kwa kweli. Je, mnaweza kufanya

hilo?

Aprili 27, 1992

Sura ya 38

Kotekote katika uzoefu wa wanadamu umbo Langu halijakuwepo, wala kuwepo kwa uongozi wa maneno Yangu, na kwa hiyo Nimemuepuka mwanadamu kwa umbali kila mara na kisha Nikaondoka kwake. Nadharau uasi wa wanadamu. Sijui kwa nini; inaonekana ni kana kwamba Nimemchukia mwanadamu tangu mwanzo, na bado Nahisi huruma kubwa kwake. Hivyo ndivyo watu daima wamekuwa na mitazamo miwili kunihusu—kwani Nampenda mwanadamu, na pia Namchukia. Ni nani kati yao ni mwenye kujali kweli upendo Wangu? Na ni nani anayejali chuki Yangu? Machoni Pangu, mwanadamu ni kitu kilichokufa, bila uhai, kama kwamba ni sanamu za udongo zinazosimama miongoni mwa vitu vyote. Wakati mwingine, kutotii kwa wanadamu huipa msukumo hasira Yangu kwao. Nilipoishi miongoni mwa wanadamu, wangenipa tabasamu hafifu Nilipofika ghafla, kwa sababu walikuwa daima wananitafuta kwa makusudi, kama kwamba Nilikuwa Nacheza nao duniani. Hawakunizingatia kwa dhati, na kwa sababu ya mtazamo wao Kwangu Sikuwa na budi ila “kustaafu” kutoka kwa “wakala” wa wanadamu. Bado, Nataka kutangaza kwamba ingawa “Nimestaafu,” “pensheni” Yangu haiwezi kupungua kwa senti moja. Kwa sababu ya “ukubwa wa cheo” Changu katika “wakala” wa wanadamu, Naendelea kudai malipo kutoka kwao, malipo ambayo Nawadai. Ingawa mwanadamu ameniacha, angeweza kuelekea fumbato Langu? Nililegeza fumbato Langu kwake kwa kiasi fulani, kumruhusu kujiingiza katika tamaa zake za mwili, na hivyo alithubutu kuwa jeuri, bila kizuizi, na inaweza kuonekana kuwa hakunipenda kweli, kwa vile aliishi katika mwili. Je, inawezekana kwamba upendo halisi unapatikana kwa malipo na mwili? Yawezekana kwamba yote Niombayo kwa mwanadamu ni “upendo” wa mwili? Kama huu kwa hakika ungekuwa ukweli, basi mwanadamu angekuwa na thamani gani? Wote ni takataka isiyo na thamani! Zisingekuwa “nguvu Zangu za mwujiza” za kudumu, Ngingekuwa Nimemwacha mwanadamu zamani sana—hata ni kwa nini kusumbuka kukaa pamoja naye na kukubali “dhuluma” ya mwanadamu? Lakini Nilivumilia. Nilitaka kufikia msingi wa shughuli za mwanadamu. Nitakapomaliza tu kazi Yangu duniani Nitapaa juu mbinguni ili kumhukumu “bwana” wa vitu vyote; hii ni kazi Yangu ya msingi, kwa maana tayari Nimemdharau mwanadamu sana. Ni nani asingemchukia adui yake? Nani asingemwangamiza adui yake? Mbinguni, Shetani ni adui Yangu, duniani, mwanadamu ni adui Yangu. Kwa sababu ya muungano kati ya mbingu na dunia, vizazi tisa vyao vinapaswa kuchukuliwa kuwa na hatia kwa ushirikiano, na hakuna atakayesamehewa. Nani aliwaambia wanipinge? Ni nani aliwaambia waniasi? Ni kwa nini mwanadamu hawezi kujifundua kwa asili yake ya kale? Kwa nini mwili

wake daima huongezeka ndani yake? Yote haya ni ushahidi wa hukumu Yangu kwa mwanadamu. Ni nani anayethubutu kutoshindwa na ukweli? Nani anayethubutu kusema hukumu Yangu imeathiriwa na hisia? Mimi ni tofauti na mwanadamu, kwa hiyo Nimeondoka kwake, kwa maana Mimi si mwanadamu hasa.

Kila kitu Ninachofanya kina madhumuni; wakati mwanadamu “anapofichua” “ukweli” Kwangu, Namsindikiza kwenye “uwanja wa kuua,” kwa kuwa hatia ya wanadamu inatosha kustahili kuadibu Kwangu. Na kwa hiyo Siwaadibu watu bila kutambua; badala yake, kuadibu Kwangu juu yao daima kunafaa ukweli wa dhambi zao. La sivyo wanadamu hawangeinama kamwe na kukubali hatia yao Kwangu kwa sababu ya uasi wao. Watu wote wanainamisha vichwa vyao kwa kusita kwa sababu ya hali ya sasa, lakini mioyo yao bado haijaridhika. Nawapa watu “bari” kunywa, na kwa hiyo viungo vyao ndani yao huonekana wazi mbele ya “lenzi”; uchafu na kinyaa ndani ya tumbo la mwanadamu bado hayajafutwa. Aina mbalimbali za uchafu hububujika kupitia mishipa yao, kwa hiyo sumu ndani yao inakua. Kwa kuwa mwanadamu ameishi namna hii kwa muda mrefu ameizoea na haioni kuwa ya ajabu. Kutokana na hilo, viini vya maradhi ndani yao hukomaa, kuwa asili yao, na kila mtu huishi chini ya utawala wao. Ndiyo sababu watu wanakimbia kila mahali kama farasi wa mwitu. Ilhali hawatambui kamwe hii; wao hutikisa tu kichwa kuashiria kukubali. Ukweli ni kwamba mwanadamu hatilii neno Langu maanani. Kama angelichukua neno langu kama dawa, basi “angefuata amri za daktari,” na angeruhusu dawa itibu ugonjwa ndani yake. Hata hivyo, moyoni Mwangu, mwenendo wake hauwezi kutimiza tamaa hii, na hivyo Naweza tu “kusalimu amri,” na kuendelea kuongea naye. Kama anasikia au la, Ninafanya tu wajibu Wangu. Mwanadamu hayuko radhi kufurahia baraka Zangu na angepitia maumivu makali ya jahanamu, hivyo siwezi kufanya chochote zaidi kuliko kukubali ombi lake. Hata hivyo, ili jina Langu na Roho Wangu visiaibishwe jahanamu, Nitamfundisha nidhamu kwanza na kisha “Nitii” matakwa yake, na kufanya hivyo ili aweze kupata “furaha ya dhati.” Siko radhi kumruhusu mwanadamu aniaibishe Mimi chini ya bendera Yangu wakati wowote au mahali popote, ndiyo maana Namfundisha nidhamu mara kwa mara. Bila kizuizi cha maneno makali Ninayonena, mwanadamu angewezaje kusimama mbele Yangu leo? Je, watu hawaepuki dhambi tu kwa sababu wanaogopa Nitaondoka? Je, si kweli kwamba hawalalamiki tu kwa sababu wanaogopa kuadibu? Ni mapenzi ya nani ambayo ni kwa ajili ya mpango Wangu tu? Watu wote wanadhani kwamba Mimi ni uungu unaokosa “ubora wa akili,” lakini ni nani anayeweza kuelewa kwamba Naweza kubaini kila kitu katika ubinadamu? Ni kama wanavyosema watu kabisa, “Kwa nini kugonga msumari kwa nyundo kubwa?” Mwanadamu “ananipenda”, si kwa sababu upendo wake Kwangu Mimi ni wa asili, lakini kwa sababu anaogopa kuadibu. Nani kati ya wanadamu alizaliwa akinipenda? Kuna yeyote hunitendea Mimi jinsi wanavyotendea mioyo yao? Na kwa hiyo Najumlisha hili na neno la hekima kwa

ulimwengu wa binadamu: Miongoni mwa wanadamu, hakuna yeyote anayenipenda.

Kwa vile Nataka kukamilisha kazi Yangu duniani, Nimeharakisha mwendo wa kazi Yangu kwa njia hii ili mwanadamu asije akarushwa mbali na Mimi, mbali sana kiasi cha kuanguka ndani ya bahari isiyo na mipaka. Ni kwa sababu Nimemwambia uhalisi wa mambo mapema ndio maana amejihadhari kwa kiasi fulani. Isingekuwa kwa ajili ya hili, ni nani angeweza kuinua matanga anapokuwa karibu kukabiliwa na upepo mkali na mawimbi? Watu wote wanafanya kazi ya kuwa macho. Ni kama kwamba Nimekuwa “jambazi” machoni pao. Wanaogopa kwamba Nitawanyang’anya vitu vyote vilivyo ndani ya nyumba zao, na hivyo wote wanasukuma “milango” yao kwa nguvu zote wanazoweza kukusanya, wakiwa na hofu kubwa sana kwamba Nitaingia ghafla. Ninapowaona wakiwa na tabia kama panya wenye hofu, Naondoka kimya. Katika mawazo ya wanadamu, inaonekana kuwa “ufunuo” unakuja ulimwenguni, na kwa hiyo wote wanakimbia kwa mchafukoge, wakitishwa sana. Ni wakati huo tu ndio Naweza kuona pepo wakizurura duniani. Sina budi ila kucheka, na katikati ya sauti ya kicheko Changu mwanadamu anashangaa na kuogopa. Hapo ndipo Natambua ukweli, na kwa hiyo Nazuia tabasamu Yangu, na Sikagui dunia tena, badala yake Narudia mpango Wangu wa awali. Sitawachukulia tena wanadamu kama mfano ambao hutumikia kama sampuli ya utafiti Wangu, kwa sababu wao ni masalio tu. Mara tu Ninapowatupa, hawana matumizi yoyote tena—wao ni chembe za taka. Wakati huu, Nitawaondoa kabisa na kuwatupa motoni. Katika akili ya mwanadamu, hukumu Yangu, uadhamu, na ghadhabu vina rehema Yangu na wema Wangu. Lakini hajui hata kidogo kwamba Nimeipuuza udhaifu wake kwa muda mrefu, na kwamba Nilifuta rehema Yangu na huruma Yangu kitambo sana, na ndiyo maana yuko katika hali waliyo ndani sasa. Hakuna mtu anayeweza kunijua, wala hawezi kuyaelewa maneno Yangu au kuuona uso Wangu, wala hawezi kufahamu maana ya mapenzi Yangu. Je, hii siyo hali ya sasa ya mwanadamu? Basi, mtu anawezaje kusema kuwa Nina huruma au wema? Sijali kuhusu udhaifu wake, na Sizingatii kasoro zake. Je, hii bado ni rehema Yangu na huruma? Na bado ni upendo Wangu kwake? Watu wote wanafikiria Mimi nasema manemo matupu ya kupendeza kwa hiyo hawaamini maneno Ninayosema. Lakini ni nani anayeelewa “Kwa kuwa hii ni enzi tofauti rehema na huruma Zangu hazipo sasa; lakini Mimi daima ni Mungu Afanyaye Anavyosema”? Mimi Niko miongoni mwa wanadamu, na katika akili za watu wananiona kama Aliye Juu Zaidi, na kwa hiyo mwanadamu anaamini kwamba Napenda kusema kwa kutumia hekima Yangu. Hivyo, mwanadamu daima huchukulia neno Langu kwa shaka. Lakini ni nani anayeweza kuelewa sheria zinazounga mkono hotuba Yangu? Nani anayeweza kuelewa asili ya maneno Yangu? Nani anayeweza kufahamu kile Ninachotaka kufanikisha kwa kweli? Nani anaweza kuelewa utondoti wa hitimisho la mpango Wangu wa usimamizi? Nani anayeweza kuwa msiri Kwangu? Katika vitu vyote, ni nani isipokuwa Mimi anayeweza kuelewa ni nini hasa Ninachofanya? Na ni nani anayeweza kujua

Sura ya 39

Kila siku Natembea juu ya ulimwengu, Nikiangalia kwa makini vitu vyote vilivyoumbwa kwa mkono Wangu. Juu ya mbingu ni mahali Pangu pa pumziko, na chini yake ni nchi ambayo Natembea. Natawala kila kitu miongoni mwa vitu vyote, Naamuru kila kitu miongoni mwa vitu vyote, Nikisababisha vyote vilivyoko kufuata hali halisi ya maisha na kutii amri ya asili. Kwa sababu Nawadharau wale wasiotii, na Nawachukia sana wale wanaonipinga na wasiojiunga na aina yao wenyewe, Nitafanya kila kitu kiutii utaratibu Wangu, bila kupinga, na zaidi ya yote Nitafanya kila kitu ndani ya ulimwengu kiwe na mpango. Nani bado anathubutu kunipinga apendavyo? Ni nani anayethubutu kutotii utaratibu wa mkono Wangu? Mwanadamu anawezaje kupenda hata kidogo kuasi dhidi Yangu? Nitawaleta watu mbele ya “babu” zao, Nitawafanya babu zao wawaongoze kurudia jamii zao, na hawataruhusiwa kuasi dhidi ya babu zao na kurudi upande Wangu. Huo ni mpango Wangu. Leo, Roho Wangu anatembea kutoka upande mmoja hadi upande mwingine wa dunia, akigawa tarakimu kwa aina zote za watu, akiweka alama tofauti kwa kila aina ya mtu, ili babu zao waweze kuwaongoza kwa ufanisi kurudia jamii zao na Sihitaji kuendelea “kuwa na wasiwasi” kuwahusu, ambalo linasumbua sana; hivyo, Nagawa kazi pia, na kusambaza juhudi. Hii ni sehemu ya mpango Wangu, na haiwezi kuvurugwa na mtu yeyote. Nitawachagua wawakilishi wanaofaa kutoka katika kila kilichoko ili kusimamia vitu vyote, na kusababisha unyenyekevu wa mpango wa wote walio mbele Yangu. Mimi mara nyingi huzurura juu ya mbingu, na mara nyingi Hutembea chini yake. Nikiitazama dunia kuu ambayo watu huja na kwenda ndani, Nikiwaangalia kwa makini wanadamu, walivyojaa juu ya dunia, na Nikiona ndege na wanyama wanaoishi juu ya sayari, Sina budi kuwa na hisia kubwa moyoni Mwangu. Kwa sababu, wakati wa uumbaji, Niliumba vitu vyote, na ukamilifu wa kila kitu kinatekeleza wajibu wake katika nafasi yake chini ya utaratibu Wangu, Mimi hucheka kutoka juu, na wakati ambapo vitu vyote chini ya mbingu husikia sauti ya kicheko Changu, hivyo mara moja hutiwa moyo, kwani wakati huu shughuli Yangu kubwa hukamilika. Naongeza hekima ya mbinguni ndani ya mwanadamu, kumfanya aniwakilishe miongoni mwa vitu vyote, kwani Nilimuumba mwanadamu ili awe mwakilishi Wangu, sio kunipinga Mimi bali kunisifu katika kina cha moyo wake. Na ni nani awezaye kutimiza maneno haya rahisi? Kwa nini daima mwanadamu hujihifadhia moyo wake? Je, moyo wake si Wangu? Sio kwamba Nataka vitu kutoka kwa mwanadamu bila ya masharti, lakini kwamba yeye daima amekuwa Wangu. Ningewezaje bila mpango kuwapatia wengine vitu ambavyo ni Vyangu? Ningewezaje kutoa “nguo” ambazo Nimezitengeneza kwa mtu mwingine kuvaa? Katika macho ya watu, ni kana

kwamba Nimepoteza akili Yangu, Nikiugua ugonjwa wa akili, na Sielewi chochote kuhusu njia za binadamu, ni kama kwamba Mimi ni mpumbavu. Na kwa hiyo, watu daima huniona kuwa mnyofu, lakini hawanipendi kwa dhati. Kwa sababu yote ambayo mwanadamu anafanya ni kwa ajili ya kunidanganya kwa makusudi, Nawakomesha wanadamu wote kwa hasira. Miongoni mwa vitu vyote Nilivyoumba, wanadamu pekee ndio hujaribu kila mara kubuni njia za kunicheza shere, na ni kwa sababu ya hili ndio Nasema kwamba mwanadamu ni “mtawala” wa vitu vyote.

Leo, Nawatupa watu wote katika “tanuru kubwa” ili wasafishwe. Nasimama juu kuangalia kwa makini watu wakichomeka motoni na, kwa kulazimishwa na miale ya moto, watu wanatoa ukweli. Hii ni mojawapo ya njia ambazo kwazo Mimi Hufanya kazi. Kama haingekuwa hivyo, watu wangekiri kuwa “wanyenyekevu,” na hakuna mtu ambaye angependa kuwa wa kwanza kufungua mdomo wake kuzungumza juu ya uzoefu wake mwenyewe, lakini wote wangeangaliana tu. Hili hasa ndilo dhihirisho la hekima Yangu, kwa kuwa Niliamua mapema mambo ya leo kabla ya enzi. Hivyo, watu wanaingia ndani ya tanuru bila kujua, kama kwamba wameongozwa huko kwa kamba, kama kwamba wamekuwa wasiosikia. Hakuna mtu anayeweza kuepuka shambulio la ndimi za moto, wao “wanashambuliana,” “wanakurupuka huku na huko wakifurahia,” bado wakihangaika juu ya hatima yao wenyewe katika tanuru, wakiogopa sana kwamba watateketea hadi kufa. Ninapochochea moto, unakuwa mkubwa mara moja, ukitapakaa mbinguni, na miale yake hukwama kwa majoho Yangu mara kwa mara, kama kwamba inajaribu kuyavuta katika tanuru. Watu wananiangalia kwa macho yaliyokodoa. Mara moja, Naufuata moto ndani ya tanuru, na wakati huu, miale ya moto inaongezeka, na watu wanalia. Nazurura kati ya ndimi za moto. Miale ya moto inazidi, lakini haina nia ya kunidhuru, na Ninatoa majoho yaliyo juu ya mwili Wangu kwa miale ya moto mara nyingine—lakini inakaa mbali na Mimi. Wakati huo tu ndio watu wanaona wazi uso Wangu halisi kwa nuru ya miale ya moto. Kwa sababu wako kati ya joto kali la tanuru, wanakimbia kuelekea pande zote kwa sababu ya uso Wangu, na tanuru inanza “kuchemka” mara moja. Wote walio katika miale ya moto wanamwona Mwana wa Adamu, ambaye amesafishwa katika ndimi za moto. Ingawa mavazi yaliyo juu ya mwili Wake ni ya kawaida, ni ya uzuri mkubwa kabisa; ingawa viatu vilivyo katika miguu Yake si vya ajabu, vinachochea wivu mkubwa; mng’aro mkali unaangaza kutoka kwa uso Wake, macho Yake yanang’aa, na inaonekana kuwa ni kwa sababu ya nuru iliyo machoni Mwake ndio watu wanaona uso wake halisi kwa dhahiri. Watu wanaingiwa na hofu, na wanaona vazi jeupe juu ya mwili Wake, na nywele Zake, nyeupe kama sufu, zinaning’inia chini kuelekea kwa mabega Yake. Kwa kutambulika, mshipi wa dhahabu juu ya kifua chake unaangaza kwa nuru ya kupofusha, huku viatu vilivyo katika miguu Yake ni vya kuvutia zaidi. Na kwa kuwa viatu vinavyovaliwa na Mwana wa Adamu vinabaki katikati ya moto, watu wanaamini kuwa ni vya ajabu. Ni wakati wa milipuko ya maumivu tu ndio watu huona kinywa cha Mwana wa

Adamu. Ingawa wako kati ya usafishaji wa moto, hawaelewi maneno yoyote kutoka kwa kinywa cha Mwana wa Adamu, na hivyo, wakati huu, hawasikii lolote zaidi kuhusu sauti ya kupendeza ya Mwana wa Adamu, lakini wanaona upanga mkali ukiwa ndani ya kinywa Chake, na Hasemi zaidi, lakini upanga Wake unamuumiza mwanadamu. Wakiwa wamezingirwa na miale ya moto, watu wanavumilia maumivu. Kwa sababu ya udadisi wao, wanaendelea kutazama umbo la ajabu la Mwana wa Adamu, na ni wakati huu tu ndio wanagundua kuwa nyota saba katika mkono Wake zimepotea. Kwa sababu Mwana wa Adamu yuko ndani ya tanuru, na sio hapa duniani, zile nyota saba katika mkono wake zinaondolewa, kwa maana ni sitiera tu. Wakati huu, hazitajwi tena, lakini zinagawanywa kwa sehemu mbalimbali za Mwana wa Adamu. Katika kumbukumbu za watu, kuwepo kwa nyota saba kunaleta kero. Leo, mimi Sifanyi mambo kuwa magumu kwa mwanadamu, Naondoa zile nyota saba kutoka kwa Mwana wa Adamu, na Naunganisha sehemu zote za Mwana wa Adamu kuwa kitu kizima. Ni wakati huu tu ambapo mwanadamu anaona umbo Langu lote. Watu hawatatenganisha Roho Wangu na mwili Wangu, kwa kuwa Nimepaa kutoka duniani hadi juu zaidi. Watu wameuona uso Wangu halisi, hawanitenganishi tena, na Sivumilii tena masingizio ya mwanadamu. Kwa sababu Natembea katika tanuru kubwa pamoja na mwanadamu, yeye bado ananitegemea, anahisi kuweko Kwangu katika ufahamu wake. Hivyo, yote ambayo ni dhahabu safi hukusanyika polepole pamoja nami katikati ya kuchomeka kwa moto, ambao ni wakati ule ule ambapo kila moja inaainishwa kulingana na asili. Ninabainisha kila aina ya “chuma,” Nikisababisha zote kurudi kwa jamii yake, na sasa tu ndio vitu vyote vinaanza kurudishiwa nguvu ...

Ni kwa sababu mwanadamu ana madoa mengi sana ndio Namtupa ndani ya tanuru ateketezwe. Hata hivyo hakomeshwi na miale ya moto, bali anasafishwa, ili Nipendezwe naye—kwani Ninachotaka ni kitu kilichoundwa kwa dhahabu safi, bila takataka, si vitu vichafu, vyenye najisi. Watu hawaelewi hali Yangu ya moyo, kwa hiyo kabla ya kupanda juu ya “meza ya upasuaji” wanazongwa na wasiwasi, kama kwamba, baada ya kuwachangua, Nitawaua papo hapo wanapolala juu ya meza ya upasuaji. Naelewa hali za watu za moyo, na hivyo Naonekana kuwa mshirika wa wanadamu. Nina huruma nyingi kwa “msiba” wa mwanadamu, na Sijui ni kwa nini mwanadamu “ameugua.” Kama angekuwa na afya, na bila ulemavu, kungekuwa na haja gani ya kulipa gharama, na kukaa juu ya meza ya upasuaji? Lakini ukweli hauwezi kufutwa—nani alimwambia mwanadamu asizingatie “usafi wa chakula”? Nani alimwambia asizingatie kuwa na afya? Leo, Nina njia gani nyingine? Ili kuonyesha huruma Yangu kwa mwanadamu, Naingia katika “chumba cha upasuaji” pamoja naye—na ni nani aliniambia Nimpende mwanadamu? Hivyo, Mimi binafsi Nachukua “kisu cha daktari mpasuaji” na kuanza “kufanya upasuaji” kwa mwanadamu ili kuzuia athari zozote zionekanazo baada ya kuugua. Kwa sababu ya uaminifu Wangu kwa mwanadamu, watu walilia machozi katikati ya maumivu

kuonyesha shukrani yao Kwangu. Watu wanaamini kuwa Nathamini haki, kwamba Nitasaidia wakati “marafiki” Zangu wako katika shida, na watu wanashukuru zaidi kwa ajili ya wema Wangu, na wanasema watanitumia “zawadi” ugonjwa huo utakapoponywa—lakini Sitilii maanani maneno yao, na badala yake Nalenga kumpasua mwanadamu. Kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu wa mwili, chini ya athari ya kisu yeye huyafumba macho yake na kulala juu ya meza ya upasuaji akiwa ameshtuka—lakini Sijali, Naendelea tu kufanya kazi iliyo mikononi Mwangu. Wakati upasuaji umemalizika, watu wameepuka kutoka kwa “taya za chui mkubwa mwenye milia.” Nawastawisha kwa virutubisho vingi, na ingawa hawajui, virutubisho vilivyo ndani yao huongezeka polepole. Kisha Nawatazama Nikitabasamu, na wanaona tu uso Wangu halisi kwa dhahiri baada ya kupata tena afya yao, na kwa hiyo wananipenda zaidi, wananichukulia kama baba yao—na je, huu sio uhusiano kati ya mbingu na dunia?

Mei 4, 1992

Sura ya 40

Watu hukodolea macho kila mwendo Wangu, kana kwamba Nakaribia kuleta mbingu chini, na wao kila mara hukanganyikiwa na shughuli Zangu, kana kwamba matendo Yangu ni yasiyoeleweka kabisa kwao. Hivyo, wao hufuata nyayo Zangu kwa yote watendayo, wakiogopa sana kwamba watakosea Mbinguni na kutupwa katika “ulimwengu wa wenye kufa.” Sijaribu kuwashikilia watu, ama Huufanya upungufu wao lengo la kazi Yangu. Wakati huu, wanafurahia sana, na kuja kunitegemea Mimi. Ninapotoa kwa mwanadamu, watu hunipenda Mimi jinsi wayapendavyo maisha yao wenyewe, lakini Niulizapo vitu kutoka kwao, wao hujitenga na Mimi. Ni kwa nini? Hawawezi hata kutia katika matendo “haki na akili” ya ulimwengu wa mwanadamu? Kwa nini Natoa matakwa kama hayo kwa watu tena na tena? Je, ni kweli kwamba Sina chochote? Watu hunichukulia Mimi kama mwombaji. Niombapo vitu kutoka kwao, wao hushikilia “makombo” yao mbele Yangu ili “Niyafurahie,” na hata husema wananitunza Mimi kwa njia maalum. Mimi huziangalia sura zao mbaya na vioja, na Mimi huondoka kwa mwanadamu tena. Chini ya hali kama hizi, watu husalia wasiofahamu, na huchukua tena vitu Nilivyowanyima, wakingoja kurudi Kwangu. Nimetumia wakati mwingi, na kulipa gharama kubwa, kwa ajili ya mwanadamu—lakini wakati huu, kwa sababu isiyojulikana, dhamiri za watu zimesalia zisizoweza kamwe kutekeleza shughuli zao za asili. Kutokana na hilo, Naorodhesha tashwishi zao za kuendelea kati ya “maneno ya fumbo,” kutumika kama “rejeleo” la vizazi vya baadaye, kwa sababu haya ni “matokeo ya uchunguzi wa kisayansi” yaliyozaliwa na “kazi ngumu” ya watu; Ningeyaondoaje kwa kawaida? Hii haingekuwa “kusikitisha” makusudi mazuri ya watu? Kwani Mimi, hata hivyo, Nina dhamiri, Sijishughulishi na mwanadamu katika matendo ya ujanja, ya kutapeli—je, matendo Yangu siyo hivyo? Je, hii siyo “haki na akili”

inayozungumziwa na mwanadamu? Miongoni mwa binadamu, Nimefanya kazi bila kukoma mpaka wakati wa sasa. Na kuwasili kwa nyakati kama leo, watu bado hawanijui Mimi, wao bado hunichukulia Mimi kama mgeni, na hata, kwa kuwa Nimewapeleka “ukingoni” wao hukuza chuki zaidi Kwangu. Wakati huu, upendo katika mioyo yao umetoweka kitambo bila dalili. Sijisifu, seuze kumdunisha mwanadamu. Naweza kumpenda mwanadamu milele, na pia Naweza kumchukia milele, na hili kamwe halitabadilika, kwani Nina ustahamilivu. Lakini mwanadamu hana ustahamilivu huu, yeye kila mara hughairighairi Kwangu, yeye kila mara hunisikiliza kidogo tu Nifunguapo kinywa Changu, na Nifungapo kinywa Changu na kuto sema chochote, yeye punde hupotea kati ya mawimbi ya ulimwengu mkubwa. Hivyo, Mimi hufupisha hili katika methali nyingine: Watu hukosa ustahamilivu, na hivyo hawawezi kuutimiza moyo Wangu.

Huku watu wanapoota, Nasafiri katika nchi za dunia Nikinyunyizia “harufu ya kifo” iliyo mikononi Mwangu miongoni mwa binadamu. Watu wote ghafula huacha uchangamfu na kuingia katika daraja inayofuata ya maisha ya binadamu. Miongoni mwa wanadamu, viumbe vinavyoishi haviwezi kuonekana tena, maiti imetapakaa kila mahali, vitu vinavyojawa na uchangamfu hutoweka mara moja bila dalili, na harufu ya kusonga ya maiti huenea kote ardhini. Mimi huufunika uso Wangu mara moja na kuondoka kwa mwanadamu, kwa kuwa Naanza hatua inayofuata ya kazi, kuwapa wale ambao wamekuwa hai mahali pa kuishi na kusababisha watu wote kuishi katika nchi iliyo bora. Hii ni nchi iliyobarikiwa—nchi isiyo na huzuni au kuhema kwa majonzi—Niliyomtayarishia mwanadamu. Maji yabubujikayo kutoka kwa chemchemi za bonde ni safi kabisa, meupe kabisa ya kuweza kuonekana mpaka chini, yanatiririka bila kukoma na kamwe hayakauki, watu huishi kwa upatanifu na Mungu, ndege huimba, na kati ya upepo mwanana na jua la vuguvugu, mbingu na dunia vyote ni tulivu. Leo, hapa, maiti ya watu wote imelala hapa na pale katika mchafukoge. Bila watu kujua, Naachilia ndwele yoyote yenye kufisha iliyo mikononi Mwangu, na miili ya binadamu huoza, bila kuacha dalili yoyote ya mwili kutoka utosini hadi kidoleni, na Naenda mbali sana kutoka kwa mwanadamu. Kamwe Sitakusanyika na mwanadamu tena, kamwe Sitakuja miongoni mwa binadamu, kwani hatua ya mwisho ya usimamizi Wangu wote imefika mwisho, na Sitawaumba wanadamu tena, Sitatilia maanani mwanadamu tena. Baada ya kusoma maneno kutoka kinywani Mwangu, watu wote hukosa tumaini, kwani hawataki kufa—lakini ni nani “hafi” kwa ajili ya “kuwa hai”? Ninapowaambia watu Nakosa mazingaombwe ya kuwafanya kuwa hai, wao huangua kilio kwa uchungu; kweli, ingawa Mimi ndiye Muumba, Ninayo tu nguvu ya kuwafanya watu wafe, na Nakosa uwezo wa kuwafanya wawe hai. Kwa hili, Naomba msamaha kwa mwanadamu. Hivyo, Nilimwambia mwanadamu kabla kwamba “Nina deni lake lisilolipika”—lakini alidhani Nilikuwa nakuwa mpole. Leo, na majilio ya ukweli, bado Nasema hili. Sitausaliti ukweli Ninenapo. Katika dhana zao, watu huamini kwamba kuna njia nyingi ambazo kwazo Mimi

huzungumza, kwa hiyo wao kila mara hukamata imara maneno Ninayowapa huku wakitumaini kitu kingine. Je, hizi sizo motisha zenye kosa za mwanadamu? Ni chini ya hali hizi ndiyo Nathubutu kusema “kwa ujasiri” kwamba mwanadamu hanipendi kweli. Singekana dhamiri na kupotosha ukweli, kwa kuwa Singewapeleka watu katika nchi yao iliyo bora; mwishowe, wakati ambapo kazi Yangu itaisha, Nitawaongoza katika nchi ya kifo. Kwa hiyo ni bora kabisa watu wasilalamike kunihusu—je, sio kwa sababu watu “hunipenda” Mimi? Je, sio kwa sababu shauku yao ya baraka ni ya nguvu sana? Kama watu hawangetaka kutafuta baraka, kungekuwaje na “msiba” huu? Kwa ajili ya “uaminifu” wa watu Kwangu, kwa vile wamenifuata Mimi kwa miaka mingi, wakifanya kazi kwa bidii licha ya kutotoa mchango wowote kamwe, Nawafichulia machache ya kile kinachofanyika katika chumba cha siri. Kwa vile, leo, kazi Yangu bado haijafikia kiwango fulani na watu bado hawajatupwa katika shimo la moto, Nawashauri waondoke mara wanapoweza—wote ambao watabaki wataelekea kupitia msiba na bahati kidogo, na bado hawataweza kuepuka kifo mwishowe. Nawafungulia wazi “milango ya utajiri”; yeyote ambaye yuko radhi kuondoka aanze safari mara anapoweza—kama atangoja mpaka kuadibu kufike, atakuwa amechelewa sana. Maneno haya si dhihaka—ni ukweli halisi. Maneno Yangu yanatamkwa kwa mwanadamu kwa dhamiri nzuri, na kama hamtaenda sasa, mtaenda lini? Watu kweli wanaweza kuyaamini maneno Yangu?

Sijawahi kufikiria sana kuhusu majaliwa ya mwanadamu; Mimi hufuata tu mapenzi Yangu mwenyewe, Sizuiliwi na watu. Ningeondoaje mkono Wangu kwa sababu ya woga wao? Kotekote katika mpango wa usimamizi Wangu wote, Sijawahi kamwe kufanya matayarisho zaidi kwa ajili ya matukio ya mwanadamu. Mimi hutenda tu kwa kadri ya mpango Wangu wa asili. Zamani, watu “walijitolea” wenyewe Kwangu na Sikuwa moto wala baridi kwao. Leo, wamejitoa wenyewe “sadaka” Kwangu, na Naendelea kutokuwa moto wala baridi kwao. Sijaridhika kwa sababu watu wanatoa sadaka ya maisha yao kwa ajili Yangu, wala Sijawi na furaha nyingi, bali Naendelea kuwapeleka katika eneo la uangamizi kwa mujibu wa mpango Wangu. Sitilii maanani mtazamo wao wakati wa kukiri—Moyo Wangu usio kunjufu, wa baridi ungewezaje kuguswa na mioyo ya binadamu? Je, Mimi ni mojawapo wa wanyama wenye mhemko miongoni mwa wanadamu? Mara nyingi Nimewakumbusha watu kwamba Mimi sina hisia, lakini wao hutabasamu tu, wakiadini Nakuwa mpole tu. Nimesema kwamba “Mimi sijui falsafa za maisha za ulimwengu wa mwanadamu,” lakini watu hawajawahi kufikiria hivyo, na wakasema kwamba njia ambazo kwazo Mimi hunena ni nyingi sana. Kwa sababu ya vizuizi vya dhana hii ya mwanadamu, Sijui ni kwa toni gani, na kwa njia gani, kunena na watu—na kwa hiyo, bila chaguo lingine, Naweza tu kuzungumza waziwazi na toni ya kuwaambia. Naweza kufanya nini kingine? Njia ambazo kwazo watu huzungumza ni nyingi sana—wao husema “Sitegemei hisia bali Natenda haki,” ambayo ni aina ya wito wametangaza kwa miaka mingi,

lakini hawawezi kutenda kwa mujibu wa maneno yao, maneno yao ni matupu—kwa hiyo Nasema kwamba watu hukosa uwezo kwani “maneno yao na utimilifu hutokea sawia.” Ndani ya mioyo yao, watu huamini kwamba kutenda hivyo ni kuniiga Mimi—lakini Sina haja ya uigaji wao, Nimechoshwa nao. Kwa nini watu kila mara humpinga Yule ambaye huwalisha? Je, Nimempa mwanadamu kidogo sana? Kwa nini watu kila mara humwabudu Shetani kisirisiri bila Mimi kujua? Ni kana kwamba wao hunifanyia Mimi kazi na mshahara wa kila mwezi ambao Mimi huwapa hautoshi kukidhi gharama ya maisha yao, kwa sababu hiyo wao hutafuta kazi nyingine nje ya saa za kufanya kazi ili waweze kuzidisha mara mbili ujira wao—kwani matumizi ya watu ni makubwa sana, na inaonekana hawajui namna ya kuendelea kuishi. Kama kweli ingekuwa hivyo, Ningewaambia waondoke katika “kiwanda” Changu. Zamani sana Nilimweleza mwanadamu kwamba kunifanyia Mimi kazi hakuhusishi utendewaji maalum: Bila kinzano, Mimi huwatendea watu kwa haki na kwa kweli, kwa kuchukua mfumo wa “fanya bidii pata zaidi, fanya kidogo pata kidogo, usifanye kazi yoyote hutapata chochote.” Nizungumzapo, Sifichi chochote; kama yeyote anaamini “sheria za kiwanda” Changu kuwa kali mno, anatakiwa kuondoka mara moja, Nitalipia “gharama ya usafiri” wao. Mimi ni “mwenye huruma” katika kuwashughulikia watu kama hao, Siwalazimishi kubaki. Kati ya watu hawa wasiohesabika, Singempata “mfanyakazi” ambaye anaupendeza moyo Wangu mwenyewe? Watu hawapaswi kunidharau Mimi! Kama watu bado wananiasi Mimi na watake kutafuta “ajira” mahali pengine, Sitawalazimisha—Ningelikaribisha, Sina budi! Je, sio kwa sababu Nina “sheria na kanuni” nyingi mno?

Mei 8, 1992

Sura ya 41

Wakati mmoja Nilianza shughuli kubwa miongoni mwa wanadamu, lakini hawakutambua, kwa hivyo ilinibidi Nitumie neno Langu ili kuwafichulia. Na hata hivyo, mwanadamu bado hangeweza kuyaelewa maneno Yangu, na akasalia kutojua malengo ya mpango Wangu. Na hivyo kwa sababu ya kasoro na dosari za mwanadamu, alifanya mambo ili kukatiza mpango Wangu wa usimamizi, na pepo wachafu wakachukua nafasi ya kujidhihirisha, wakawafanya wanadamu kafara wao, mpaka wakateswa na pepo hao wachafu na wakachafuliwa kila mahali. Ulikuwa wakati huu ambapo Niliona nia ya mwanadamu na kusudi lake. Nilishusha pumzi kutokana na kushindwa kuelewa: Ni kwa nini sikuzote lazima mwanadamuatende kwa ajili ya maslahi yake? Je, kuadibu Kwangu hakukusudii kumkamilisha? Je, Najaribu kumvunja moyo? Lugha ya mwanadamu ni nzuri sana, na nyororo, lakini matendo ya wanadamu ni mabaya mno. Kwa nini matakwa Yangu kwa mwanadamu kila mara huambulia patupu? Ni kana kwamba Nilikuwa Namtaka mbwa apande mti? Je, Najaribu kuleta taabu bila sababu? Ninapotekeleza

mpango Wangu wote wa usimamizi, Nimeumba “viwanja mbalimbali vya majaribio,” hata hivyo kwa ajili ya mandhari mabaya, na kwa ajili ya miaka mingi sana ya kutokuwa na mwanga wa jua, mandhari yanabadilika siku zote, yakisababisha kubomoka kwayo, na kwa hivyo katika kumbukumbu Yangu, Nimetupa viwanja vingi vya aina hii. Na bado sasa, sehemu kubwa ya mandhari inaendelea kubadilika. Kama siku moja dunia itabadilika kwa kweli kuwa aina nyingine, Nitaiweka kando bila kusita—je, hiyo si hatua ambayo Niko ndani sasa katika kazi Yangu? Lakini mwanadamu hajui hata kidogo kuhusu jambo hili; wao “wanaadibiwa” tu chini ya uongozi Wangu. Hili ni la faida gani? Je, Naweza kuwa Mungu anayekuja kwa nia tu ya kumwadibu mwanadamu? Katika mbingu, wakati mmoja Nilipanga kwamba mara tu Ninge kuwa miongoni mwa wanadamu, Ningejiunganisha nao, ili wale wote Niwapendao wangeweza kuwa karibu nami bila chochote kutugawanya. Hata hivyo, wakati huu, malalamiko yapi mwanadamu anaweza kuwa nayo? Mwanadamu anaweza kunifanyia Mimi? Je, si wanadamu ni kama panzi kwenye ukuta? Sili kwa ajili ya kutokuwapo kwao. Ni nini chaweza kufanywa? Wanadamu wote ni wachezaji wanaokubaliana na kundi. Ningewaacha wanadamu waponyoke kutoka kwa fumbato Langu, na hata zaidi Nitaweza kuwaacha warudi katika kiwanda Changu kutoka nchi za kigeni. Wakati huu, wangeweza kuwa na malalamiko gani? Mwanadamu anaweza kunifanya nini? Je, si wanadamu ni kama nyasi imeayo juu ya mlima? Na hata hivyo, Simdhuru mwanadamu kwa kosa hili, bali badala yake Nampa lishe Yangu. Nani aliwalazimisha watende kidhaifu? Nani aliwafanya wakose lishe? Naisisimua mioyo baridi ya wanadamu kwa kumbatio Langu kunjufu, nani mwingine anaweza kufanya jambo kama hilo? Kwa nini Nimeipanua kazi hii miongoni mwa wanadamu? Je, mwanadamu anaweza kuufahamu moyo Wangu kweli?

Miongoni mwa watu wote ambao Nimechagua, Nimeshiriki katika shughuli, na kwa hiyo kila mara watu wengi huja na kutoka nyumbani Kwangu kwa mtiririko usiokoma. Wote hushiriki katika kanuni mbalimbali Kwangu, kana kwamba wanajadiliana na Mimi biashara, kiasi kwamba kazi Yangu ina shughuli nyingi sana hivi kwamba wakati mwingine Sina nafasi ya kushughulikia mizozo yote ya wanadamu. Nawasihi watu wasiwe wa kuongezea mizigo Yangu; itafaa iwapo wataendesha shughuli zao wenyewe badala ya kunitegemea siku zote. Wasitende kila mara kama watoto ndani ya nyumba Yangu; hiyo ni faida gani? Kazi Yangu ni biashara kubwa. Si duka fulani la mtaani, au kijiduka. Kila mara wanadamu hukosa kufahamu na Mimi, kana kwamba wote ni watoto watundu walio na tamaa isiyotosheleza kwa michezo, hazingatii biashara ya maana kamwe, na kwa hivyo wengi hushindwa kutimiza “zoezi la kufanyia nyumbani” Ninalowapangia. Na kwa hiyo wanadamu hawa wanathubutu vipi kwenda mbele ya “mwalimu”? Kwa nini huwa hawafanyi wajibu wao asilani? Moyo wa mwanadamu ni kitu cha aina gani? Hata sasa Sielewi. Kwa nini mioyo ya wanadamu huwa inabadilika kila mara? Kama vile siku katika mwezi wa Juni, mara kwa mara jua lenye joto kali huwa katili, nyakati zingine mawingu

huwa meusi na mazito, na nyakati zingine upepo mkali huvuma. Hivyo kwa nini wanadamu hawawezi kujifunza kutokana na uzoefu wao? Labda huku ni kutia chumvi. Wanadamu hawajui kubeba mwavuli wakati wa msimu wa mvua, hivyo kwa sababu ya kutojua kwao wamelowa mara nyingi kwa kuonekana ghafula kwa mvua kutoka mbinguni, kana kwamba Nilikuwa Nawachokoza kwa makusudi na walikuwa wanavamiwa kila mara na mvua ya mbinguni. Au labda ni kwamba Mimi ni “katili” sana, Nikimfanya kila mtu kuwa msahaulifu na hivyo asiye makini, asijue la kufanya siku zote. Hakuna mwanadamu ambaye amewahi kuelewa kusudi au umuhimu wa kazi Yangu. Kwa hiyo wote hufanya kazi ya kujiletea taabu, na kujiadibu. Yawezekana kwamba Nawaadibu kwa makusudi? Kwa nini wanadamu hujiletea taabu? Kwa nini kila mara wao huingia mtegoni moja kwa moja? Mbona wasijadiliane na Mimi, lakini badala yake wao hujitafutia kazi? Yawezekana kwamba Nawapa wanadamu kidogo sana?

Nilichapisha kazi Yangu ya kwanza miongoni mwa wanadamu wote, na kazi Yangu ilipowafanya watu waipende sana, wote walikuwa makini kuisoma, na kupitia kwa masomo yao ya uzingatiaji walikuwa walipata mengi. Inaonekana kazi Yangu ni kama riwaya iliyo ngumu kueleweka, ya kustaajabisha, kama shairi la nathari lenye kusesitiza hisia, kama mazungumzo ya programu ya siasa, kama mchanganyiko wenye utata wa maarifa ya kawaida ya kiuchumi. Kwa kuwa kazi Yangu ya fahari sana, kuna maoni mengi yanayotofautiana kuihusu, na hakuna anayeweza kutoa muhtasari wa dibaji ya kazi Yangu. Ingawa mwanadamu ana ufahamu na kipaji “vilivyojipambanua”, kazi hii Yangu tu inatosha kuwakanganya mashujaa wote. Wakati wanadamu wanasema “damu yaweza kutiririka, machozi yaweza kutoka, lakini mtu hapaswi kuinamisha kichwa chake kwa aibu,” wao wanainamisha vichwa vyao kwa aibu bila kujua, kwa kuonyesha kujisalimisha kwao kwa kazi Yangu. Kutokana na masomo yanayotokana na uzoefu, mwanadamu amefanya muhtasari wa kazi Niliyoandika kana ni kitabu cha mbinguni ambacho kimeanguka kutoka angani. Isitoshe, Namsihi sana mwanadamu asiwe mwenye wepesi wa kuhisi. Kwa maoni Yangu, yote ambayo Nimesema ni ya kawaida sana; hata hivyo, Natumai kwamba kutoka kwa Ensiklopedia ya Maisha katika kazi Yangu, watu wanaweza kupata njia ya riziki, na kutoka kwa Hatima ya Mwanadamu, waweze kupata maana ya uzima, na kutoka kwa Siri za Mbinguni, waweze kupata mapenzi Yangu, na kutoka kwa Njia ya Wanadamu, wanaweza kugundua ustadi wa kuishi. Je, hili halingekuwa hata bora zaidi? Simlazimishi mwanadamu; kwa wale ambao hawana haja na kazi Yangu, “Nitawalipa” kwa ajili ya kitabu Changu, pamoja na “gharama ya huduma.” Simfanyi mwanadamu atende kwa kusita. Kama mwandishi wa kitabu hiki, tumaini Langu tu ni kwamba wasomaji wataipenda kazi Yangu, lakini kile ambacho watu hufurahi huwa tofauti kila mara. Kwa hiyo Nawasihi sana wanadamu wasitie matatani matarajio yao ya siku za baadaye kwa ajili ya kujiepusha na aibu. Kama huo ungekuwa ukweli, Ningewezaje, jinsi Nilivyo mwenye huruma, kustahamili aibu kama hiyo? Kama mnapenda kazi

Yangu, Natumai kwamba mtanipa mapendekezo yenu wenyewe ya thamani, ili Niweze kuendeleza uandishi Wangu, na hivyo kupitia kwa makosa ya mwanadamu Niendeleze maudhui ya uandishi Wangu. Hili linamfaidi mwandishi na msomaji, au sio? Sijui kama hili linaweza kufikiriwa kuwa sahihi. Labda kwa njia hii Naweza kuzidisha ubora wa uwezo Wangu wa kuandika, au labda kuimarisha urafiki kati yetu. Kwa jumla, Natumai kwamba wote wanaweza kushirikiana na kazi Yangu, bila pingamizi, ili maneno Yangu yaweze kuenezwa kwa kila familia na nyumba, na ili watu wote duniani waweze kuishi kati ya neno Langu. Hili ndilo lengo Langu. Natumai kwamba kupitia kwa Sura inayohusu Uzima katika maneno Yangu watu wote wanaweza kupata kitu, kama vile kanuni za maisha, au ufahamu wa makossa ambayo mwanadamu anakabiliana nayo katika ulimwengu wa wanadamu au ni nini Ninachohitaji kutoka kwa mwanadamu, au “siri” za watu wa ufalme wa leo. Hata hivyo, Nawasihi sana wanadamu waangalie Kashfa za Mwanadamu Leo; haya yanaweza kuwa ya manufaa kwa wote. Unaweza pia kusoma Siri ya Karibuni Zaidi, ambayo yanaweza kuwa hata ya manufaa zaidi kwa maisha ya watu. Pia kuna Mada Motomoto—Je, haya si ya manufaa hata zaidi kwa maisha ya watu? Hakuna madhara katika kutumia ushauri Wangu, na kuona kama una athari yoyote, na kunielezea vile mnahisi baada ya kuyasoma, ili Niweze kuandika maagizo ya matumizi ya dawa sahihi, ambayo mwishowe inaweza kukomesha kabisa magonjwa ya wanadamu. Sijui vile mapendekezo Yangu yatafanya kazi, lakini Natumai kwamba mnaweza kuyatumia kama marejeleo. Mnafikiriaje?

Mei 12, 1992

Sura ya 42

Punde tu kazi mpya inapoanza, watu wote wanakuwa na kuingia kupya, na wanasonga mbele nami bega kwa bega, tunatembea pamoja kwenye barabara kubwa ya ufalme, na kuna urafiki mkubwa kati ya mwanadamu na Mimi. Ili kuonyesha hisia Zangu, ili kudhihirisha mtazamo Wangu kwa mwanadamu, Nimemzungumzia mwanadamu kila mara. Sehemu ya maneno haya, hata hivyo, yanaweza kuwaumiza watu, huku mengine yanaweza kuwa ya msaada mkubwa kwao, na kwa hiyo Nawashauri watu kusikiliza mara kwa mara kwa manaeno yanayotoka kinywani Mwangu. Matamko Yangu huenda yasiwe sanifu na yenye ustarabu, lakini yote ni maneno kutoka kina cha moyo Wangu. Kwa kuwa binadamu ni rafiki Yangu, Nimeendelea kutekeleza kazi Yangu miongoni mwa wanadamu, na mwanadamu, pia, anafanya kila awezalo kushirikiana nami, akiogopa sana kuikatiza kazi Yangu. Wakati huu, moyo Wangu umejaa furaha kuu, kwani Nimeipata sehemu ya watu, na kwa hiyo “biashara” Yangu haiko tena katika hali ya kuporomoka, si maneno matupu tena, na “soko Langu la bidhaa maalum” halifanyi kwa uvivu tena. Watu wana akili hata hivyo, wote wako radhi “kujitolea” kwa ajili ya jina Langu

na utukufu Wangu, na kwa njia hii pekee ambapo “duka Langu la bidhaa maalum” inapata “bidhaa” zingine mpya, na kwa hiyo katika ulimwengu wa kiroho “wateja” wengi wanakuja kununua “bidhaa” Zangu. Ni wakati huu tu ndipo Napata utukufu, wakati huo tu ndipo maneno yaliyonenwa kutoka kinywani Mwangu si maneno matupu tena. Nimekuwa mshindi, na Nimerudi kwa ushindi, na watu wote wananisherehekea. Ili kuonyesha upendo wake Kwangu, ili kuonyesha kwamba linakubali kushindwa chini ya magoti Yangu, wakati huu joka kubwa jekundu linakuja pia “kusherehekea,” nami Natukuzwa kwa hili. Tangu wakati wa uumbaji mpaka leo, Nimepigana vita vingi vya ushindi, nami Nimefanya mambo mengi ya ajabu. Wakati mmoja watu wengi walinisherehekea, na kunisifu, na kunichezea dansi. Ingawa haya yalikuwa maonyesho ya kulisimua, na yasiyosahaulika, Sikuonyesha tabasamu Yangu kamwe, kwani Nilikuwa bado Sijamshinda mwanadamu, na Nilikuwa Nafanya tu sehemu ya kazi inayofanana na uumbaji. Leo si kama na wakati uliopita. Natoa tabasamu katika kiti cha enzi, Nimemshinda mwanadamu, na watu wote wanainama kwa ibada mbele Yangu. Watu wa leo si wale wa wakati uliopita. Ni wakati gani ambapo kazi Yangu haijakuwa kwa ajili ya wakati huu? Ni wakati gani ambapo haijakuwa kwa ajili ya utukufu Wangu? Kwa ajili ya kesho yenye matumaini, Nitaeleza waziwazi kazi Yangu yote ndani ya mwanadamu mara nyingi, ili utukufu Wangu wote “utulie” ndani ya mwanadamu, aliyeumbwa. Nitaichukua hii kuwa kanuni ya kazi Yangu. Wale ambao wako radhi kushirikiana nami, huiuka na kufanya bidii ili utukufu Wangu mwingi uweze kuijaza anga. Huu ndio wakati wa mtu kutumia vizuri sana vipaji vyake. Wale wote ambao wako chini ya utunzaji na ulinzi wa upendo Wangu wana nafasi ya kutumia uwezo wao hapa, mahali Pangu, na Nitavishawishi vitu vyote “kugeuka” kwa ajili ya kazi Yangu. Ndege wanaopuruka angani ni utukufu Wangu angani, bahari zilizo juu ya dunia ni mambo Yangu juu ya dunia, utawala wa vitu vyote ni onyesho Langu miongoni mwa vitu vyote, nami Natumia kila kilichoko juu ya dunia kama rasilimali ya usimamizi Wangu, na kuvifanya vitu vyote kuzidisha, kusitawi, na kujawa na uhai.

Wakati wa uumbaji, Nilikuwa tayari Nimeamua kwamba kazi Yangu duniani itakamilika katika enzi ya mwisho. Wakati ambapo kazi Yangu itaisha ndio hasa wakati ambapo mambo Yangu yote yatadhihirishwa katika anga. Nitawafanya watu walio duniani wakubali mambo Yangu, na mbele ya “kiti cha hukumu,” matendo Yangu yatathibitishwa, ili yakubalike miongoni mwa watu walio kote duniani, ambao watasalimu amri. Hivyo, baadaye, Nitaanzisha shughuli ambayo haijawahi kamwe kutekelezwa katika enzi zilizopita. Tangu leo na kuendelea, Nitatoa waziwazi matendo Yangu hatua kwa hatua, ili hekima Yangu, ajabu Yangu, na kutoeleweka Kwangu vitakubaliwa na kuthibitishwa katika kila eneo la jamii. Hasa, vyama vyote vinavyotawala duniani vitafanywa kukubali zaidi kwa matendo Yangu, kiasi kwamba mambo Yangu yatahukumiwa na “mahakimu,” na “kutetewa” na “mawakili,” na hivyo mambo Yangu

yatakubaliwa, na kusababisha watu wote kuinamisha vichwa vyao na kusalimu amri. Tangu wakati huu na kuendelea, matendo Yangu yatatambuliwa na kila eneo la jamii, na huu utakuwa wakati ambapo Nitapata utukufu wote duniani. Katika wakati huo, Nitamwonekana mwanadamu na Sitajificha tena. Wakati huu, matendo Yangu bado hayajafika kilele. Kazi Yangu inaendelea mbele, na wakati ambapo itafika kilele chake ndio wakati ambapo itamalizika. Nitawashinda kabisa watu wa mataifa yote, Nitasababisha wanyama wakali wageuke kuwa wa kuweza kufugwa kama wanakondoo mbele Yangu, na Nitasababisha joka kubwa jekundu kutii mbele Yangu kama watu walio duniani. Nitawashinda adui zangu wote mbinguni, na Nitasababisha washindani Wangu wote duniani kushindwa. Huu ni mpango Wangu, na ajabu ya matendo Yangu. Mwanadamu anaweza tu kuishi chini ya ushawishi wa asili chini ya uongozi Wangu—hawezi kufanya uamuzi wake mwenyewe! Ni nani anaweza kuuponyoka mkono Wangu? Nimeainisha asili yote, na kuisababisha kuwapo katikati ya sheria, na ni kwa sababu ya hili tu ndipo duniani kuna sheria kama vile uvuguvugu wa majira ya kuchipua na ubaridi wa majira ya kupukutika kwa majani. Madhumuni ya maua yaliyo duniani kunyauka wakati wa majira ya baridi na kuchanua wakati wa majira ya joto ni kwa sababu ya ajabu ya mkono wa Wangu, madhumuni ya bata bukini kupuruka kwenda kusini wakati wa majira ya baridi ni kwa sababu Narekebisha halijoto, na madhumuni ya bahari kunguruma ni kwa sababu Nataka kuvizamisha majini vitu vilivyo juu ya ardhi. Ni kipi kisichopangwa na Mimi? Tangu wakati huu na kuendelea, “uchumi wa asili” wa mwanadamu unashindwa kabisa kwa maneno Yangu, na watu hawakomeshi tena kuwapo Kwangu kwa sababu ya kuweko kwa “sheria asilia.” Ni nani atawahi tena kana kuweko kwa Mtawala wa vitu vyote? Mbinguni, Mimi ni Mkuu; miongoni mwa vitu vyote, Mimi ni Bwana; na miongoni mwa watu wote, Mimi ni wa kwanza. Ni nani anayethubutu kulifunika hili kwa “rangi”? Je, uwongo ungeweza kuvuruga kuweko kwa ukweli? Katika nafasi hii ya thamani, Naanza kwa mara nyingine kazi iliyo mikononi Mwangu, Sikubali tena kuingilia kwa mwanadamu, Nikidumisha kuzunguka kwa mitambo.

Nimeongeza “viungo” mbalimbali kwenye maneno Yangu, na hivyo itaonekana kana kwamba Mimi ni mmoja wa wapishi wakuu wa wanadamu. Ijapokuwa watu hawajui jinsi ya kutumia viungo, wanaifurahia ladha yake; wakiwa wameshika “sahani,” wote wanafurahia “vyakula” ambavyo Nimetayarisha. Sijui ni kwa nini, watu kila mara hutaka kula zaidi vyakula ambavyo Mimi Hutayarisha binafsi. Ni kana kwamba wao hunistahi sana, kana kwamba wao huniona Mimi kuwa kiungo cha hali ya juu sana kati ya vyote, na hawajali kabisa kuhusu wengine. Kwa sababu Najiheshimu sana, Sitaki kuvunja “bakuli la chuma la wali” la wengine kwa madhumuni Yangu mwenyewe. Hivyo, Nachukua nafasi ya kuondoka jikoni na Nawapa wengine nafasi ya kujibainisha. Ni kwa namna hii tu ndipo moyo Wangu uko thabiti; Sitaki kuwafanya watu wanitegemee na kuwadharau wengine, hiyo si sawa. Ni nini thamani ya kuwa na cheo ndani ya

mioyo ya watu? Je, kweli Mimi ni mwingi wa ufidhuli na Asiye na mantiki hivyo? Je, kweli Niko radhi kutaka cheo? Kama ni hivyo, basi kwa nini Naanzisha shughuli kubwa kama hiyo? Sitaki kung’ang’ania umaarufu na bahati dhidi ya wengine, Nadharau umaarufu na bahati ya kidunia, hilo silo Ninalofuatilia. Simchukulii mwanadamu kama mfano mwema wa kuigwa, Sipigani wala kupokonya, lakini Napata riziki kwa kutegemea “ustadi” Wangu, nami Sifanyi matendo ya kupita kiasi. Hivyo, wakati ambapo Natembea kila mahali duniani, Natenda kwanza na kudai “malipo ya kazi ya mikono” baadaye—hii pekee ndiyo haki na maana inayozungumziwa na mwanadamu, hakuna kutia chumvi katika hili, halijapunguzwa hata kidogo, Nazungumza kulingana na maana ya asili ya ukweli. Natembea kwenda mbele na nyuma miongoni mwa wanadamu, Nikitafuta wale ambao ni wenye haki na wa maana, lakini hakujakuwa na matokeo. Na kwa kuwa watu wanapenda kupiga bei, ama bei ni ya juu sana au ya chini sana, na kwa hiyo bado Nafanya wajibu ulio mikononi Mwangu. Leo, bado Sijui ni kwa nini mwanadamu hazingatii wajibu wake, kwa nini hajui jinsi kimo chake kilivyo kikubwa. Watu hata hawajui kama kimo chao kina uzani gramu kadhaa au liang^[a] kadhaa. Na hivyo, bado wao wananirairai. Ni kana kwamba kazi Yangu yote imekuwa bure, kana kwamba maneno Yangu ni mwangwi ndani ya milima mpana, na hakuna ambaye amewahi kutambua asili ya maneno na matamko Yangu. Na kwa hiyo Natumia hili kama msingi wa kufanya muhtasari wa methali ya tatu: Watu hawanijui, kwa kuwa hawanioni. Ni kana kwamba, wakiwa wamekula maneno Yangu, watu wanakunywa dawa fulani ili kusaidia mmeng’enywa wa chakula, na kwa sababu athari za dawa hiyo ni kubwa sana, wanapoteza kumbukumbu, na kwa hiyo maneno Yangu yanakuwa kile kinachosahaulika, mahali Nilipo panakuwa pembe wanayoisahau, na kwa ajili ya hili Ninatanafusi. Kwa nini Nimefanya kazi nyingi sana, lakini hakuna thibitisho lake ndani ya watu? Je, kwani Sijatia bidii ya kutosha? Au ni kwa sababu Sijaelewa kile ambacho mwanadamu anahitaji? Nimepungukiwa na mawazo katika hili, chaguo Langu pekee ni kutumia amri Zangu za utawala ili kuwashinda watu wote. Sitakuwa tena mama mwenye upendo, bali Nitawasimamia wanadamu wote kama baba mkali!

Mei 15, 1992

Tanbihi:

a. “Liang” ni kipimo cha uzito cha Uchina, liang moja ni gramu 50.

Sura ya 43

Labda ni kwa sababu tu ya amri Zangu za utawala ndio watu “wamevutiwa sana” na maneno Yangu. Wasingaliongozwa na amri Zangu za utawala, wote wanalikuwa wakilia kama chui wakubwa wenye milia ambao wamesumbuliwa sasa hivi. Kila siku Mimi Huzurura juu ya

mawingu, Nikiwaangalia binadamu wanaoifunika dunia wakiwa katika kukurukakara zao, wakizuiliwa na Mimi kwa njia ya amri Zangu za utawala. Kwa njia hii jamii ya binadamu inawekwa kwa hali ya utaratibu, na hivyo Ninadumisha amri Zangu za utawala. Kuanzia wakati huu na kuendelea, wale walio duniani wanapokea kila aina za kuadibu kwa sababu ya amri Zangu za utawala, na kuadibu huku kunapowashukia wanadamu wote husababisha ghasia kubwa na kukimbia kila upande. Wakati huu, mataifa ya dunia yanaangamia mara moja, mipaka kati ya taifa na taifa inaacha kuwepo, mahali hapagawanyiki tena, na hakuna kitu cha kumtenganisha mwanadamu kutoka kwa mwanadamu. Naanza kufanya “kazi ya kiitikadi” katikati ya binadamu, ili watu waweze kuishi pamoja kwa amani mmoja kwa mwingine, bila kupigana tena, na, Ninapowaambatanisha watu na kuanzisha uhusiano miongoni mwa wanadamu, watu wanaungana. Nitajaza mbingu na maonyesho ya kazi Yangu, ili kila kitu kilicho chini ya ardhi kisujudu chini ya nguvu Zangu, Nikitekeleza mpango Wangu wa “umoja wa ulimwengu” na kusababisha hili tamanio Langu moja kufaulu, na ili binadamu wasiweze “kuzurura kote” juu ya uso wa dunia lakini wapate hatima ya kufaa bila kuchelewa. Naifikiria jamii ya binadamu kwa kila njia, Nikifanya hilo ili kwamba wanadamu wote waje kuishi katika nchi ya amani na furaha hivi punde, ili siku za maisha yao zisiwe na huzuni na ukiwa tena, na ili mpango Wangu hautakuwa bure duniani. Kwa kuwa mwanadamu yupo pale, Nitalijenga taifa Langu duniani, kwani sehemu ya maonyesho ya utukufu Wangu iko duniani. Juu mbinguni, Nitaiweka miji Yangu kwenye haki na hivyo kufanya kila kitu kiwe kipya juu na chini. Nitaleta yote yaliyopo juu na chini ya mbingu kuwa katika umoja, ili vitu vyote duniani viungane na vyote vilivyo mbinguni. Huu ndio mpango Wangu, ndio Nitakaoutimiza katika enzi ya mwisho—mtu asiingilie sehemu hii ya kazi Yangu! Kupanua kazi yangu katika nchi za Mataifa ni sehemu ya mwisho ya kazi Yangu duniani. Hakuna anayeweza kuelewa kazi Nitakayoifanya, na hivyo watu wamepumbazwa kabisa. Na kwa sababu Nina shughuli nyingi za kazi Yangu duniani, watu huchukua fursa hiyo “kufanya mzaha.” Ili kuwazuia kuwa watundu sana, Nimewaweka chini ya kuadibu Kwangu kwanza ili wastahamili nidhamu ya ziwa la moto. Hii ni hatua moja katika kazi Yangu, nami Nitatumia uwezo wa ziwa la moto kutimiza kazi hii Yangu, la sivyo haitawezekana kutekeleza kazi Yangu. Nitawafanya wanadamu ulimwenguni kote kutii mbele ya kiti Changu cha enzi, Nikiwagawanya katika makundi mbalimbali kulingana na hukumu Yangu, Nikiwaainisha kulingana na makundi haya, na kuwaainisha zaidi katika jamii zao, ili binadamu wote wakome kuniasi, badala yake waingie katika mpango mzuri na wa taratibu kulingana na makundi ambayo Nimeyataja—mtu yeyote asitembee huku na huko bila kufikiria! Katika ulimwengu wote, Nimefanya kazi mpya; katika ulimwengu wote, binadamu wote hutunduwa na kupigwa na bumbuwazi kwa kuonekana Kwangu kwa ghafla, upeo wao wa macho ulibubujika kwa namna ambayo haijawahi kutendeka awali kwa ajili ya kuonekana Kwangu wazi. Je, leo haiko hivi hasa?

Nimechukua hatua ya kwanza na kuanzisha sehemu ya kwanza ya kazi Yangu kati ya mataifa yote na watu wote. Sitavuruga mpango wangu wa kuanza upya: Utaratibu wa kazi miongoni mwa nchi za Mataifa umeanzishwa kwa mujibu wa taratibu za kazi Yangu mbinguni. Wakati wanadamu wote wanayainua macho yao ili kuangalia kila ishara na kitendo, huo ndio wakati ambapo Natupa ukungu duniani. Macho ya wanadamu yanafilizwa mara moja, wasiweze kupata mwelekeo wowote, kama kondoo katika mbuga la jangwa, na, wakati dhoruba kali inapoanza kuvuma, vilio vyao huzamishwa na mvumo wa upepo mkali. Kati ya mawimbi ya upepo, umbo za binadamu zinaweza kuonekana kwa uhafifu, lakini hakuna sauti ya binadamu inaweza kusikika—ingawa wanadamu wanapiga kelele kwa sauti kubwa mno, jitihada hiyo ni bure. Wakati huu, binadamu hulilia na kuomboleza kwa sauti kubwa, wakitumaini kwamba mwokozi atashuka ghafla kutoka angani ili kuwaongoza nje ya jangwa lisilo na mipaka. Lakini, haijalishi imani yao ni kubwa kiasi gani, mwokozi habanduki, na matumaini ya mwanadamu yanavunjika: Moto wa imani ambao umewashwa unazimwa kwa dhoruba kutoka jangwani, na mwanadamu analala kifudufudi katika eneo kame na lisilokaa watu, asiweze kamwe kuinua mwenge unaong'aa, na anazirai pasipo hisia.... Ninapotumia nafasi hiyo Nasababisha mahali penye raha kuonekana mbele ya macho ya mwanadamu. Lakini, wakati moyo wake huenda ukawa na furaha kubwa, mwili wa mwanadamu ni dhaifu sana kukubali, akilala akiwa mlegevu katika kila ncha; hata ingawa anaona matunda mazuri yanayokua katika mahali penye raha, anakosa nguvu ya kuyachuma, kwa sababu “rasilimali za ndani” za mwanadamu zimemalizwa zote mpaka hakuna chochote kilichosalia ndani yake. Mimi Huchukua vitu ambavyo mwanadamu anahitaji na kumpatia, lakini yeye hutabasamu kwa muda mfupi tu, uso wake ukiwa hauna furaha kabisa: Kila sehemu ndogo ya nguvu za binadamu imetoweka isionekane tena, ikitoweka juu ya hewa inayosonga. Kwa sababu hii, uso wa mwanadamu hauonyeshi hisia kabisa, ni mwali mmoja tu wa upendo unaong'aa kutoka katika macho yake mekundu, na upole mkarimu kama ule wa mama akimwangelia mtoto wake. Mara kwa mara, midomo ya mwanadamu iliyo mikavu iliyopasuka, hupigapiga, kana kwamba inakaribia kuzungumza lakini haina nguvu ya kufanya hivyo. Nampa mwanadamu maji kidogo, lakini anatikisa kichwa chake tu. Kutokana na vitendo hivi visivyo vya kawaida na visivyotabirika, Nafahamu kwamba mwanadamu tayari amepoteza tumaini lolote katika nafsi yake mwenyewe, na ananiangalia tu kwa mtazamo wa maombi katika macho yake, kama kwamba anaomba kitu fulani. Lakini, bila kujua desturi na maadili ya wanadamu, Nastaajabishwa na maonyesho ya uso na matendo ya binadamu. Ni wakati huu tu ndipo Nagundua ghafla kuwa siku za kuwepo kwa mwanadamu zinakaribia mwisho wake haraka, na Namwelekezea mtazamo wa huruma. Na ni wakati huu tu ndipo mwanadamu anaonyesha tabasamu ya kufurahia, akiniashiria kwa kichwa chake, kama kwamba amelipa kila tamani lake. Binadamu hawana huzuni tena; duniani, watu hawalalamikii tena ukiwa wa uhai, na huacha shughuli zote na “maisha.” Kutoka hapo, hakutakuwa na tanafusi

tena duniani, na siku ambazo jamii ya binadamu itaishi zitajawa na furaha ...

Nitaziondoa shughuli za binadamu kwa njia inayostahili kabla ya kujishughulisha na kazi Yangu Mwenyewe, binadamu wasije wakaendelea kuingilia kazi Yangu. Shughuli za mwanadamu sio dhamira Yangu kuu, shughuli za wanadamu hazina mpango kabisa. Kwa sababu roho ya mwanadamu ni ndogo sana—inaonekana kuwa binadamu hawataki kuonyesha rehema hata kwa chungu, au kwamba chungu ni adui wa wanadamu—daima kuna rabsha inayoendelea kati ya wanadamu. Ninaposikiliza rabsha ambayo wanadamu wanafanya, Naondoka mara nyingine na kutozingatia hadithi zao zaidi. Katika macho ya binadamu, Mimi ni “kamati ya wakazi,” Nikiwa mtaalamu katika kusuluhisha “migogoro ya familia” kati ya “wakazi.” Watu wanapokuja mbele Yangu, wao siku zote huja na sababu za kibinafsi na, kwa shauku kubwa, hueleza “uzoefu wao wenyewe usio wa kawaida,” wakiongeza maoni yao wenyewe kadri wanavyoendelea. Naangalia mwenendo wa binadamu usio wa kawaida: Nyuso zao zimefunikwa kwa vumbi—vumbi ambalo, chini ya “umwagiliaji” wa jasho, linapoteza “uhuru” wake linapounda mchanganyiko na jasho kwa haraka, ili nyuso za wanadamu “zirutubishwe” zaidi, kama mchanga pwani kando ya bahari, ambapo nyayo zinaweza kuonekana mara chache. Nywele zao zinafanana na vivuli vya wafu, havina mng’aro, zinazosimama wima kama vipande vya majani yaliyosakama katika mviringo. Kwa sababu hasira yake ni kali sana, kufikia kiwango ambapo yeye mwenyewe amejitia ghadhabu kubwa, uso wake unatoa “mvuke” hapa na pale, kama “ghadhabu” ya jasho. Nikimchunguza kwa karibu, Naona kwamba uso wa mwanadamu umefunikwa kwa “miale” kama jua kali, ndiyo sababu kuna mawingu ya gesi ya moto inayoinuka kutoka kwake, nami Nina wasiwasi sana kwamba hasira yake inaweza kuuchoma uso wake, ingawa yeye mwenyewe hajali. Kwa hali ya mambo yalivyo, Namsihi mwanadamu kufifiza hasira yake kidogo, kwa maana hili lina faida gani? Kwa nini awe hivi? Kwa sababu ya kuwa na hasira, mabua ya majani makavu juu ya uso wa “mviringo” huu yanateketezwa hasa kwa mielele ya jua; katika hali kama hii, hata “mwezi” unageuka kuwa mwekundu. Namsihi mwanadamu apunguze hasira yake—ni muhimu kuilinda afya yake. Lakini mwanadamu hasikilizi ushauri Wangu; badala yake, anaendelea “kutoa malalamiko” Kwangu—ina maana gani? Hakika sio kwamba ukarimu Wangu hautoshi kwa raha ya binadamu? Au kwamba anakataa kile Ninachompa? Kwa hasira ya ghafla, Naigeuza meza, ambapo mwanadamu hathubutu kusimulia tena matukio yoyote ya kisisimua kutoka kwenye hadithi yake na, akiwa na hofu Nisije Nikamwelekeza kwenye “jela” ili kungojea kwa siku chache, anachukua fursa iliyosababishwa na hamaki Yangu ili kuponyoka. La sivyo, mwanadamu hangeweza kuwa tayari kuyaacha mambo kwa muda, lakini angeendelea kuchacharisha kwa kujipigia domo mwenyewe—Nimechoshwa Ninaposikia hivyo. Ni kwa nini binadamu ni wenye utata sana ndani ya mioyo yao? Yawezekana kuwa Nimeweka sehemu nyingi sana za “vipuri” katika umbo la

mwanadamu? Kwa nini yeye daima hujifanya mbele Yangu? Hakika si kwamba mimi ni “mwelekezi” wa azimio la “migogoro ya kiraia”? Je, Nilimtaka mwanadamu aje Kwangu? Hakika Mimi si hakimu wa mkoa? Kwa nini mambo kati ya watu daima yanaripotiwa Kwangu? Tumaini Langu ni kwamba mwanadamu ataona haja ya kuchukua jukumu la nafsi yake mwenyewe na kutoniingilia, kwa sababu Nina kazi nyingi sana ya kufanya.

Mei 18, 1992

Sura ya 44

Watu huichukulia kazi Yangu kama kijalizo, hawaachilii chakula au usingizi kwa ajili yake, na kwa hiyo Sina budi ila kufanya madai yafaayo kwa mwanadamu kama inavyostahili mtazamo wake Kwangu. Nakumbuka kuwa wakati mmoja Nilimpa mwanadamu neema nyingi sana na baraka nyingi, lakini baada ya kunyakua vitu hivi aliondoka mara moja. Ilikuwa ni kama kwamba Nilikuwa Nampa bila kufahamu. Na kwa hiyo, mwanadamu amenipenda Mimi daima kati ya dhana zake mwenyewe. Nataka mwanadamu anipende kweli, lakini leo, watu bado wanasitasita, wasiweze kunipa upendo wao wa kweli. Katika mawazo yao, wao huamini kwamba iwapo watanipa upendo wao wa kweli, wataachwa bila chochote. Ninapopinga, miili yao yote hutetemeka—lakini wao hubaki kutotaka kutoa upendo wao wa kweli Kwangu. Ni kama kwamba wanasubiri kitu fulani, na hivyo wanatazama mbele, wasiniambie kamwe ukweli wa kile kinachoendelea. Ni kama kwamba vinywa vyao vimebanwa na kijikaratasi cha gundi, kwa hivyo matamko yao yanayumbayumba daima. Nimekuwa bepari wa kikatili. Watu daima huniogopa: Wanaponiona, wao hupotea mara moja wasionekane tena, wakihofu juu ya kile Nitawauliza kuhusu hali zao. Sijui sababu ya watu kuweza kuwa na upendo wa kweli kwa “wanakijiji wenzao,” lakini hawawezi kunipenda, ambaye ni mwadilifu katika roho. Kwa sababu ya hili Nashusha pumzi: Kwa nini watu daima huachia huru upendo wao katika ulimwengu wa mwanadamu? Kwa nini Siwezi kuonja upendo wa mwanadamu? Je, ni kwa sababu Mimi si mmoja wa wanadamu? Watu daima huntendea Mimi kama nduli katika milima. Ni kama kwamba Nakosa kile kinachomkamilisha mtu wa kawaida, na kwa hiyo mbele Yangu watu daima hujisingizia toni ya maadili ya juu. Mara nyingi hunikokota mbele yao kunikemea, wakinikaripia kama wanavyomfanyia mtoto wa umri wa kwenda shule ya chekechea; kwa sababu, katika kumbukumbu za watu, Mimi ni mtu asiye na mantiki na asiye na elimu, wao daima huchukua jukumu la mwalimu mbele Yangu. Siwaadibu watu kwa kasoro zao, bali Nawapa msaada ufao, kuwaruhusu kupokea “msaada wa kiuchumi” wa mara kwa mara. Kwa kuwa mwanadamu daima ameishi katikati ya janga na huona vigumu kutoroka, na katikati ya msiba huu daima ameniita, Mimi huwasilisha “riziki ya nafaka” bila kuchelewa katika mikono yake, kuwaruhusu watu wote kuishi katika jamii kubwa ya enzi mpya, na kupitia wema wa jamii

kubwa. Ninapochunguza kwa makini kazi miongoni mwa wanadamu, Natambua kasoro nyingi za mwanadamu, na kutokana na hilo Nampa mwanadamu msaada. Hata wakati huu, bado kuna umasikini wa kipekee miongoni mwa wanadamu, na hivyo Nimetoa huduma ifaayo kwa “maeneo masikini,” kuyainua kutoka kwa umasikini. Hii ni njia ambayo Mimi hufanyia kazi, kuruhusu watu wote kufurahia neema Yangu kadri wanavyoweza.

Watu hapa duniani hupitia kuadibu bila kufahamu, na kwa hiyo Nafungua mkono Wangu mkubwa na kuwavuta upande Wangu, kuwaruhusu bahati nzuri ya kufurahia neema Yangu duniani. Duniani, ni kitu gani kisicho tupu na bila thamani? Natembea miongoni mwa sehemu zote katika ulimwengu wa mwanadamu, na ingawa kuna majengo mengi maarufu na mazingira asili ya kupendeza, kila mahali Niendapo kwa muda mrefu pameondolewa uhai. Wakati huo tu ndipo Ninahisi huzuni na ukiwa duniani: Duniani, maisha yamepotea kitambo, kuna harufu ya kifo tu, na hivyo Nimewahi kumwomba mwanadamu kuharakisha na kuiacha nchi hii ya mateso. Yote Nionayo ni yenye kunukia utupu. Mimi Huchukua nafasi ya kuvurumisha maisha yaliyo mkononi Mwangu kwa wale ambao Nimewachagua; ghafla, kuna kiwanja cha kijani juu ya nchi. Watu wako radhi kufurahia vitu vya uhai juu ya dunia, lakini Sipati furaha kwa jambo hili; watu daima hutunza mambo yaliyo duniani, na kamwe hawaoni utupu wao, kiasi kuwa, baada ya kufikia kiwango hiki leo, bado hawaelewi kwa nini hakuna uhai uliopo duniani. Leo, wakati Ninapotembea katikati ya ulimwengu, watu wanaweza kufurahia neema ya mahali Nilipo, na wao huchukulia hili kama rasilimali, wasifuatilie kamwe chanzo cha uzima. Wote hutumia kile Ninachowapa kama rasilimali, lakini hakuna hata mmoja wao anayejaribu kutekeleza kazi ya asili ya uhai. Hawajui jinsi ya kutumia au kukuza maliasili, na hivyo wanabaki masikini. Ninakaa miongo ni mwa wanadamu, Naishi miongoni mwa wanadamu, lakini leo bado mwanadamu hanijui. Ingawa watu wamenipa msaada mwingi sana kutokana na Mimi kuwa mbali sana na nyumbani, ni kama kwamba bado Sijaanzisha urafiki wa kweli na mwanadamu, na hivyo Mimi bado Nahisi ukosefu wa haki wa ulimwengu wa mwanadamu; machoni Pangu, mwanadamu, hata hivyo, ni mtupu, na hakuna hazina ya thamani yoyote kati ya mwanadamu. Sijui watu wana mtazamo gani kuhusu maisha ya binadamu, lakini kwa jumla, Wangu mwenyewe hautenganishwi na neno “tupu.” Natumai watu hawanifikirii vibaya kwa sababu ya hili—hivyo ndivyo Nilivyo tu, Mimi ni mkweli, Sijaribu kuwa wa adabu. Hata hivyo, Ningewashauri watu kuzingatia kwa makini kile Ninachofikiria, kwani maneno Yangu, hata hivyo, ni ya msaada kwao. Sijui ni ufahamu gani walionao watu kuhusu “utupu.” Tumaini langu ni kwamba watatumia juhudi kidogo kwa kazi hii. Wangefanya bora kupitia kwa kweli maisha ya binadamu, na kuona kama wanaweza kupata “madini” yoyote ya thamani ndani yake. Sijaribu kufifiza matumaini ya watu, Nataka tu wapate maarifa fulani katika maneno Yangu. Mimi daima Hukimbia huku na huko kwa ajili ya mambo ya binadamu, lakini hata baada ya kufikia kiwango

hiki leo, bado watu hawajazungumza neno la shukrani, kana kwamba wana shughuli nyingi sana, na wamesahau hili. Hata leo, Mimi bado Sijui ni matokeo gani yamepatikana kwa mwanadamu kukimbia huku na huko siku nzima. Hadi leo bado Sina nafasi katika mioyo ya watu, na kwa hiyo mara nyingine tena Nazama katika mawazo. Nimeanza kuingia katika kazi ya kuchunguza “kwa nini watu hawana moyo ambao unanipenda kweli”: Nitamwinua mwanadamu kwenye “meza ya upasuaji,” Nitaukata moyo wake vipande vipande, na kuangalia kile kinachozuia njia ndani ya moyo wake na kumzuia kunipenda kweli. Chini ya athari ya “kisu,” watu hukaza macho yao na kuyafumba, wakinisubiri Nianze, kwani wakati huu, wamesalimu amri kabisa; katika mioyo yao Napata ughushi mwingine mwingi. Katika mioyo yao, kubwa kati ya haya ni mambo ya watu wenyewe. Ingawa wanaweza kuwa na mambo machache tu nje ya miili yao, yale yaliyo ndani ya miili yao haya hesabiki. Ni kama kwamba moyo wa mwanadamu ni sanduku kubwa la hifadhi, lililojaa utajiri, kila kitu ambacho watu wangewahi kuhitaji. Wakati huo tu ndio Naelewa kwa nini watu huwa hawanijali kamwe: Ni kwa sababu wana kujitosheleza kwingi—wana haja gani ya msaada Wangu? Kwa hiyo, Naondoka kwa mwanadamu, kwani watu hawana haja ya msaada Wangu; kwa nini “Nitende bila haya” na Nipatane na karaha yao?

Nani anajua kwa nini, lakini kila mara Nimekuwa radhi kuzungumza miongoni mwa wanadamu—ni kama kwamba Siwezi kujisaidia. Na hivyo, watu wananiangalia kama Nisiye na thamani, daima wao huntendea kama kitu kisicho na thamani, hawanitendei kama kitu cha kuheshimiwa. Hawanitunzi, na hunikokota nyumbani wakati wowote na tena kunitupa nje, “wakinifunua” mbele ya umma. Nina chukizo kubwa sana kwa tabia ya mwanadamu ya aibu, na hivyo Nasema waziwazi kuwa mwanadamu hana dhamiri. Lakini watu ni wenye msimamo usiobadilika, wanachukua “panga na mikuki” yao na kupigana na Mimi, wakisema kuwa maneno Yangu ni tofauti na hali halisi, wakisema kuwa Nawasingizia—lakini Siwalipizi adhabu kutokana na tabia yao ya vurugu. Mimi hutumia tu ukweli Wangu kuwavutia watu, kuwafanya wasikie aibu wenyewe, baada ya hapo wanarudi nyuma kimyakimya. Sishindani na mwanadamu, kwani hakuna faida katika hilo. Nitashikilia wajibu Wangu, na Natumai kwamba mwanadamu anaweza pia kushikilia wajibu wake, na si kutenda dhidi Yangu. Je, isingekuwa bora kupatana kwa amani hivi? Kwa nini tumize uhusiano wetu? Tumepatana miaka hii yote—kuna haja gani kuleta taabu kwa sisi wawili? Je, hilo halitakosa manufaa kwa mojawapo ya sifa zetu? Wetu ni “urafiki wa kale” wa miaka mingi, “kufahamiana kwa zamani”—kuna haja gani kuachana kwa hali ya ukali? Je, kuna manufaa kwa hili? Natumai watu wanazingatia athari, kwamba wanajua ni nini kizuri kwao. Mtazamo wangu kwa mwanadamu leo ni wa kutosha majadiliano ya maisha na mwanadamu—kwa nini watu daima hushindwa kutambua wema Wangu? Ni kwa sababu hawana uwezo wa kujieleza? Je, wanakosa msamiati wa kutosha? Kwa nini wao daima hukosa maneno? Ni nani asiyejua jinsi Nitendavyo? Watu wanafahamu vizuri kabisa matendo Yangu. Ni vile tu

wao hupenda kutumia wengine kwa manufaa yao, kwa hivyo huwa hawako radhi kamwe kuweka kando mambo wayapendayo; ikiwa neno moja linagusa mambo wayapendayo, wanakataa kuachilia mpaka wawe wamepata udhibiti—na kuna haja gani katika hilo? Badala ya kushindana juu ya kiasi gani wanachoweza kutoa, watu hushindana juu ya kiasi gani wanaweza kupata. Ingawa hakuna furaha katika cheo chao, wanakitunza sana, na hata kukiona kama hazina ya thamani kubwa sana—na hivyo heri wavumilie kuadibu Kwangu kuliko kuacha baraka za cheo. Watu hujiona sana, na hivyo huwa kamwe hawako radhi kujiweka kando. Pengine kuna upungufu fulani mdogo katika tathmini Yangu ya mwanadamu, au Nimeweka alama juu yake ambayo si kali wala ya upolelakini, kwa jumla, matumaini Yangu ni kwamba watu walichukue hili kama onyo.

Mei 21, 1992

Sura ya 45

Wakati mmoja Nilichagua bidhaa nzuri kubaki ndani ya nyumba Yangu, ili ndani yake kungekuwa na utajiri usio na kifani, na ingepambwa hivyo, Nilipata raha kutokana na hilo. Lakini kwa sababu ya mtazamo wa mwanadamu Kwangu, na kwa sababu ya motisha za watu, Sikuwa na budi ila kuiweka kazi hii kando na kufanya kazi nyingine. Nitatumia motisha za mwanadamu kufanikisha kazi Yangu, Nitashawishi vitu vyote vinihudumie, na kusababisha nyumba Yangu kutokuwa ya kusunoneka na ya ukiwa tena kama matokeo. Wakati mmoja Nilitazama miongoni mwa wanadamu: Chote kilichokuwa cha mwili na damu kilikuwa katika mzubao, hakuna hata kitu kimoja kilipitia baraka ya kuweko Kwangu. Watu huishi katikati ya baraka lakini hawajui jinsi walivyobarikiwa. Kama baraka Zangu kwa wanadamu hazingekuweko mpaka leo, nani miongoni mwa wanadamu angeishi mpaka wakati huu na kukosa kuangamia? Kwamba mwanadamu anaishia ni baraka Yangu, na linamaanisha anaishi katikati ya baraka Zangu, kwa sababu hapo mwanzo hakuwa na chochote, kwa kuwa hapo mwanzo hakuwa na rasilimali ya kuishi katikati ya mbingu na dunia; leo Naendelea kumsaidia mwanadamu, na ni kwa sababu ya hili tu ndio mwanadamu anasimama mbele Yangu, akibahatika ya kutosha kuepuka kifo. Watu wamejumuisha siri za kuweko kwa mwanadamu, lakini hakuna mtu ambaye ametambua kwamba hii ni baraka Yangu. Kutokana na hili, watu wote wanalaani udhalimu ulio ulimwenguni, wote wanalalamika kunihusu kwa sababu ya kutokuwa na furaha ndani ya maisha yao. Kama si baraka Zangu, nani angeona leo? Watu wote hulalamika kunihusu kwa sababu hawawezi kuishi katikati mwa faraja. Kama maisha ya mwanadamu yangekuwa yenye kung'aa na machangamfu, kama “dharuba ya vuguvugu ya ghafula ya majira ya kuchipua” ingeingizwa ndani ya moyo wa mwanadamu, isababishe furaha isiyo na kifani ndani ya mwili wake wote, ikimwacha bila maumivu hata kidogo, basi nani

miongoni mwa wanadamu angekufa akilalamika? Nina tatizo kubwa kupata uaminifu kamili wa mwanadamu, kwani watu wana hila nyingi sana za ujanja—za kutosha, kweli kabisa, kukanganya mtu. Lakini Niletapo upinzani kwao, wao hunidharau, hawanisikilizi, kwani upinzani Wangu umegusa nafsi zao, ukiwawacha bila uwezo wa kuadilishwa kutoka utosini hadi wayoni, na hivyo watu huchukia sana kuweco Kwangu, kwani kila mara Mimi hupenda “kuwatesa.” Kwa sababu ya maneno Yangu, watu huimba na kucheza, kwa sababu ya maneno Yangu, wao hushusha vichwa vyao kwa ukimya, na kwa sababu ya maneno Yangu, wao huangua kilio. Katika maneno Yangu, watu hukata tamaa, katika maneno Yangu, wao hupata nuru ya kuendelea kuishi, kwa sababu ya maneno Yangu, wao hugaagaa na kugeuka, bila usingizi mchana na usiku, na kwa sababu ya maneno Yangu, wao huenda kasi kila mahali. Maneno Yangu huwatumbukiza watu ndani ya Kuzimu, kisha huwatumbukiza katika kuadibu—lakini, bila kulitambua, watu hufurahia baraka Zangu pia. Je, hili laweza kutimizwa na mwanadamu? Lingeweza kupatikana kama malipo ya juhudi za kutochoka za watu? Ni nani anaweza kuepuka mipango ya maneno Yangu? Hivyo, kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu, Ntoa maneno Yangu kwa wanadamu, kusababisha kasoro za mwanadamu kusitawishwa kwa sababu ya maneno Yangu, kuleta utajiri usio na kifani katika maisha ya wanadamu.

Mimi mara kwa mara Huchunguza maneno na vitendo vya watu. Katika mienendo yao na sura zao, Nimegundua “siri” nyingi. Katika kuingiliana kwa watu na wengine, “mbinu za siri” kwa utendaji huchukua nafasi muhimu sana—na hivyo, Ninaposhirikiana na mwanadamu, Nipatacho ni “mbinu za siri za kuingiliana kwa mwanadamu,” ambalo huonyesha kwamba mwanadamu hanipendi. Mimi mara kwa mara humkemea mwanadamu kwa sababu ya kasoro zake, lakini Siwezi kupata uaminifu wake. Mwanadamu hayuko radhi kuniacha Nimchinje, kwani katika “mbinu za siri za kuingiliana kwa mwanadamu” za mwanadamu, haijawahi kamwe kugunduliwa kwamba mwanadamu amepatwa na msiba wa mauti—yeye amepitia tu vipingamizi vichache katika nyakati za taabu. Watu hulika kwa sababu ya maneno Yangu, na maombi yao kila mara huwa na manung’uniko kuhusu ukatili Wangu. Ni kana kwamba wote wanatafuta “upendo” Wangu wa kweli kwa mwanadamu—lakini wangepata kupata upendo Wangu katika maneno Yangu makali? Kutokana na hilo, wao kila mara hukata tamaa kwa sababu ya maneno Yangu. Ni kana kwamba, punde tu wasomapo maneno Yangu, wao huona “mvunaji wa roho za wafu,” na hivyo hutetemeka kwa hofu. Hili hunifanya Nikose raha: Kwa nini watu wa mwili, ambao wanaishi katikati ya kifo, kila mara huogopa kifo? Je, mwanadamu na kifo ni maadui wakali? Mbona hofu ya kifo kila mara husababisha huzuni ndani ya watu? Kote kote katika matukio “yasiyo ya kawaida” ya maisha yao, wao hupitia tu kiasi kidogo cha kifo? Mbona, katika kile wasemacho, watu daima hulalamika kunihusu? Hivyo, Nafanya muhtasari wa methali ya nne ya maisha ya mwanadamu: Watu hunitii kiasi kidogo tu, na hivyo wao kila mara hunichukia. Kwa

sababu ya chuki ya mwanadamu, Mimi huondoka mara kwa mara. Kwa nini lazima Nipitie hili? Kwa nini lazima Nichochee chuki ndani ya watu kila mara? Kwa vile watu hawafurahii kuweco Kwangu, kwa nini lazima Niishi bila aibu ndani ya nyumba ya mwanadamu? Sina budi ila kuchukua “mzigo” Wangu na kumwacha mwanadamu. Lakini watu hawawezi kuvumilia kuniacha Niende, hawataki kamwe kuniacha Niondoke, wao huomboleza na kumamia, wakiwa na woga mwingi kwamba Nitaondoka, na hivyo watapoteza wanachotegemea ili kuishi. Nionapo kukaza macho kwao kwa kusihi, moyo Wangu huwa wenye huruma. Katikati ya bahari za ulimwengu, nani anaweza kunipenda? Mwanadamu amefunikwa kwa maji machafu, amemezwa na nguvu za bahari. Nachukia sana ukaidi wa mwanadamu, lakini pia Naona huruma kwa ajili ya taabu zote za wanadamu—kwani mwanadamu, hata hivyo, bado ni mwathiriwa. Naweza je kumtupa mwanadamu ndani ya maji wakati ambapo yeye ni mnyonge na mdhaifu? Je, Mimi ni mkatili hivyo kiasi cha kumpiga teke akiwa chini? Je, moyo Wangu ni katili sana? Ni kwa sababu ya mtazamo Wangu kwa wanadamu ndio mwanadamu huingia katika enzi hii ubavuni Mwangu, ni kwa sababu ya hili ndio amepitia mchana na usiku huu usio wa kawaida pamoja na Mimi. Leo, watu wako katika maumivu makubwa ya furaha, wana ufahamu mkuu wa upendo Wangu, na wanapipenda kwa nguvu nyingi, kwa sababu kuna uhai katika maisha yao, nao hukoma kuwa wana wapotevu wanaozurura mpaka kwa miisho ya dunia.

Katika siku Zangu za kuishi na mwanadamu, watu hunitegemea, na kwa sababu Namjali mwanadamu katika mambo yote, na ni mwangalifu sana katika kumtunza, watu kila mara huishi katika kumbatio Langu kunjufu, wakikosa kustahimili upepo wowote uvumao, mvua inyeshayo, au jua lichomalo; watu huishi kati ya furaha, na kunichukulia kama mama mwenye upendo. Watu ni kama maua yaliyo ndani ya nyumba ya kioo ya kuhifadhi mimea, wasioweza kabisa kuhimili mvamio wa “maafa ya asilia,” wasiweze daima kusimama imara. Hivyo Nawaweka katikati ya majaribio ya bahari zivumazo, na hawana budi ila “kuyumbayumba” bila kukoma, hawana kabisa nguvu za kupinga—na kwa vile kimo chao ni dhaifu sana na miili yao ni minyonge sana, Nahisi mzigo. Hivyo, bila kutambua hilo, watu hupitia majaribio Yangu, kwa sababu wao ni wadhaifu sana, na hawawezi kuhimili upepo unaovuma na jua lichomalo. Je, hii si kazi Yangu ya wakati huu? Kwa nini, wakati ambapo wanakabiliwa na majaribio Yangu, watu daima hububujika machozi. Je, Nawatendea udhalimu? Je, Nawachinja kwa makusudi? Kwa nini hali ya mwanadamu ambayo ni ya kupendeka hufa, isiweze kufufuliwa kamwe? Watu daima huninyakua na hawaachilii; kwa sababu hawajawahi kuweza kuishi wenyewe, kila mara wamejiruhusu kuongozwa na mkono Wangu, wakiogopa sana kuchukuliwa na mtu mwingine. Je, maisha yao yote hayaongozwi na Mimi? Wakati wa maisha yao yenye ghasia, wanapovuka milima na mabonde, wamepitia misukosuko mingi sana—je, hili halikutoka mkononi Mwangu? Kwa nini watu hawawezi kamwe kuuelewa moyo Wangu? Kwa nini nia Zangu nzuri kila mara

hueleweka vibaya na wao? Kwa nini kazi Yangu haiwezi kuendelea kwa ufanisi duniani? Kwa sababu ya unyonge wa mwanadamu, Nimejitenga na mwanadamu kila mara, ambalo hunijaza huzuni: Kwa nini hatua Yangu inayofuata ya kazi isiweze kutekelezwa na mwanadamu? Hivyo, Nanyamaza, Nikimhakiki kwa makini: Mbona kila mara Mimi huzuiwa na kasoro za mwanadamu? Kwa nini huwa kuna vizuizi kwa kazi Yangu kila mara? Leo, bado Sijapata jibu kamili katika mwanadamu, kwani mwanadamu kila mara hughairighairi, yeye si wa kawaida kamwe, ama ananichukia kabisa, au ana upendo mkubwa sana Kwangu. Mimi, Mungu Mwenyewe wa kawaida, Siwezi kustahimili mateso kama hayo kutoka kwa mwanadamu. Kwa sababu watu kila mara huwa si wa kawaida kiakili, Mimi inavyoonekana Namwogopa mwanadamu kidogo, na kwa hiyo kutazama kila mwendo wake hunifanya Nifikirie kuhusu kutokuwa kawaida kwake. Nimegundua bila kusudi siri iliyo ndani ya mwanadamu: Inadhihirika kwamba kuna mwanzilishi nyuma yake: kutokana na hilo, watu kila mara ni wakakamavu na wenye kujiamini, kana kwamba wamefanya kitu fulani kinachostahiki. Hivyo, watu kila mara hujifanya kuwa mtu mzima na humbembeleza “mtoto mdogo.” Nitazamapo kitendo cha uongo cha mwanadamu, Sina budi ila kughadhibishwa: Kwa nini watu hawajipendi na hukosa kujiheshimu hivyo? Kwa nini wasijijue? Je, maneno Yangu yamekufa? Je, maneno Yangu ni adui wa mwanadamu? Kwa nini, wanaposoma maneno Yangu, watu hukuza chuki Kwangu? Kwa nini watu huongeza mawazo yao kwa maneno Yangu kila mara? Je, Mimi ni asiye na huruma sana kwa mwanadamu? Watu wote wanapaswa kufikiri sana kuhusu hili, kuhusu kilicho ndani ya maneno Yangu.

Mei 24, 1992

Sura ya 46

Sijui jinsi watu wanavyoendelea katika kuyafanya maneno Yangu kuwa msingi wa kuweko kwao. Nimehisi wasiwasi kila mara kwa ajili ya majaliwa ya mwanadamu, lakini watu hawaonekani kuwa na fahamu yoyote kuhusu hili—na kutokana na hilo, hawajawahi kuyatilia maanani mambo Yangu, na hawajawahi kukuza kuabudu kokote kwa ajili ya mtazamo Wangu kuhusiana na mwanadamu. Ni kana kwamba walitupa hisia zamani ili kuuridhisha moyo Wangu. Nikikumbwa na hali kama hizo, Nakimya mara nyingine. Kwa nini maneno Yangu hayastahili kufikiriwa na watu, kuhusu kuingia zaidi? Je, ni kwa sababu “Sina uhalisi” nami Najaribu kuwa na mamlaka juu ya watu? Kwa nini watu kila mara “hunitendea kwa njia ya pekee”? Je, Mimi ni mgonjwa aliye katika wadi yake pekee maalum? Kwa nini, mambo yakiwa yamefika kiwango ambacho yamefika leo, bado watu huwa na maoni tofauti kunihusu? Je, kuna kosa katika mtazamo Wangu kwa watu? Leo, Nimeanza kazi mpya juu ya ulimwengu. Nimewapa watu walio duniani mwanzo mpya, na Nimewaambia wote watoke nyumbani Mwangu. Na kwa kuwa

kila mara watu hupenda kujideka, Nawashauri wajijue, na wasiisumbue kazi Yangu kila mara. Katika “nyumba ya wageni” ambayo Nimeifungua, hakuna kinachotia msukumo chuki Yangu kuliko mwanadamu, kwa sababu kila mara watu huniletea taabu na kunisikitisha. Mwenendo wao huniletea aibu na Sijawahi kuweza kujiamini. Hivyo, Nazungumza nao kwa utulivu, Nikiwataka waondoke nyumbani Kwangu haraka iwezekanavyo na waache kula chakula Changu bila kukilipia. Kama wanataka kubaki, basi lazima wapitie mateso na kuvumilia kuadibu Kwangu. Katika mawazo yao, Sifahamu na Siyajui mambo yao kabisa, na hivyo kila mara wamesimama wima mbele Yangu, bila ishara yoyote ya kuanguka, wakijifanya tu kuwa wanadamu ili kukamilisha idadi. Ninapowahitaji kufanya mambo fulani, wao hushangaa: Hawakuwa wamewahi kufikiri kwamba Mungu, ambaye Amekuwa mwenye ukarimu na mwenye huruma kwa miaka mingi sana, Angeweza kusema maneno kama hayo, maneno ambayo ni ya kikatili na yasiyothibitika, na kwa hiyo wao huduwaa. Nyakati kama hizo, Naona kwamba chuki iliyo ndani ya mioyo ya watu Kwangu imekua mara nyingine, kwa sababu wameanza tena kazi ya kulalamika. Wao kila mara huilaumu dunia na kulaani Mbinguni. Lakini katika maneno yao, Sioni chochote kinachowalaani wao wenyewe kwa sababu wanajipenda sana. Hivyo Nafanya muhtasari wa maana ya maisha ya mwanadamu: Kwa kuwa watu wanajipenda kupita kiasi, maisha yao yote ni ya uchungu na matupu, na wao hujiletea uharibifu wa kujitakia maishani mwao kwa sababu ya chuki yao Kwangu.

Ingawa kuna “upendo” usiosimuliwa katika maneno ya mwanadamu kwa ajili Yangu, Ninapoyapeleka maneno haya katika “maabara” kwa ajili ya upimaji na kuyachunguza chini ya hadubini, yote yaliyo ndani yake hufichuliwa kwa uwazi kabisa. Wakati huu, Naja miongoni mwa wanadamu ili niwaruhusu waone “rekodi zao za matibabu,” ili kuwafanya waridhike kwa kweli. Watu wanapoziona, nyuso zao hujaa huzuni, wao huhisi majuto ndani ya mioyo yao—na wao hata wao huwa na wasiwasi sana kiasi cha kuwa na hamu ya kuzitelekeza njia zao za uovu na kurudi kwa njia sahihi ili kunifanya Nifurahi. Ninapoonu uamuzi wao, Nafurahishwa kabisa, Najawa na furaha: “Duniani, ni nani pasipo mwanadamu ambaye angeweza kushiriki nami furaha na huzuni? Je, si ni mwanadamu pekee?” Lakini Ninapoondoka, watu huchana rekodi zao za matibabu na kuzitupa sakafuni kabla ya kuondoka kwa mikogo. Katika hizi siku tangu wakati huo, Nimeona machache katika matendo ya watu ambayo yanaupendeza moyo Wangu. Hata hivyo uamuzi wao mbele Yangu umeongezeka mno, na, Ninapotazama uamuzi wao, Nahisi kuchukizwa, kwani ndani yao hakuna kitu kinachoweza kuwa mfano wa kufurahia Kwangu, wametiwa doa kupita kiasi. Wanapoonu Ninapuuza uamuzi wao, watu huwa baridi. Baadaye, wanatuma tu “maombi” kwa nadra kwa sababu moyo wa mwanadamu haujawahi kusifiwa mbele Yangu na umewahi tu kukataliwa nami—hakuna tena msaada wowote wa kiroho katika maisha ya watu, na kwa hiyo ari yao hupotea, na Sihisi tena kwamba hali ya hewa ni “yenye joto kali.”

Watu huteseka sana kotekote katika maisha yao, kiasi kwamba, kwa majilio ya hali ya leo, wanateswa sana nami kiasi kwamba wanakaribia kufa; kwa hiyo, nuru kutoka kwa nyuso zao inafifia, na wanapoteza “kuisimuka” kwao kwani wote “wamekomaa.” Siwezi kuvumilia kuona hali ya watu ya kusikitisha wanaposafishwa wakati wa kuadibu—lakini ni nani anaweza kumwokoia mwanadamu katika hali yake ya kushindwa? Ni nani anayeweza kumwokoia mwanadamu kutokana na maisha ya mwanadamu yenye taabu? Kwa nini watu hawajawahi kamwe kujinasua kutoka kwa lindi kuu la bahari ya mateso? Je, Mimi huwanasa watu mtegoni kwa makusudi? Watu hawajawahi kamwe kuelewa hali Yangu ya moyo, kwa hiyo Naomboleza kwa ulimwengu kwamba miongoni mwa vitu vyote mbinguni na duniani, hakuna kitu ambacho kimewahi kuutambua moyo Wangu, hakuna kitu ambacho kinanipenda kweli. Hata leo, bado Sijui kwa nini watu hawawezi kunipenda. Wanaweza kunipa mioyo yao, wanaweza kutoa hatima yao kama dhabihu kwa ajili Yangu, lakini ni kwa nini hawawezi kunipa upendo wao? Je, hawana Ninachotaka? Watu wanaweza kupenda kila kitu isipokuwa kunipenda Mimi—kwa hiyo mbona wasinipende? Ni kwa nini upendo wao daima umefichwa? Kwa nini, kwa kuwa wamesimama mbele Yangu mpaka leo, Sijawahi kamwe kuuona upendo wao? Je, hiki ni kitu wanachokosa? Je, Nafanya mambo kuwa magumu kwa watu kwa makusudi? Je, bado wana haya ndani ya mioyo yao? Wanaogopa kumpenda mtu mbaya, na kutoweza kujirekebisha? Ndani ya watu kuna siri nyingi zisizoeleweka, na hivyo Mimi daima huwa “mwenye haya na mwoga” mbele ya mwanadamu.

Leo, wakati wa kusonga mbele kuelekea kwa lango la ufalme, watu wote wanaanza kuendelea mbele—lakini wanapofika mbele ya lango, Nafunga lango, Nawafungia watu nje, na kuwataka waonyeshe pasi zao za kuingia. Kitendo cha ajabu kama hiki hakifanani na kile ambacho watu walikuwa wanatarajia, na wote wanastaajabu. Mbona lango—ambalo kila mara limekuwa wazi kabisa—leo limefungwa ghafla kwa kubanwa? Watu wanakanyaga miguu yao kwa nguvu na kutembea hapa na pale. Wanafikiri kwamba wanaweza kuingia ndani kwa hila, lakini wanaponipa pasi zao za kuingia zisizo halisi, Nazitupa ndani ya shimo la moto papo hapo—na, wanapoona “juhudi zao za kujitahidi” zikiteketea moto, wanakata tamaa. Wanashika vichwa vyao, wakilia, wakitazama mandhari mazuri ndani ya ufalme lakini wasiweze kuingia. Lakini Siwaruhusu kuingia kwa sababu ya hali yao ya kusikitisha—ni nani awezaye kuuvuruga mpango Wangu apendavyo? Je, baraka za siku za baadaye hutolewa kwa kubadilishana na ari ya watu? Je, maana ya kuweko kwa mwanadamu inategemea kuingia katika ufalme Wangu apendavyo mtu? Je, Mimi ni duni sana? Kama sio maneno Yangu makali, je, si watu wasingekuwa wameingia katika ufalme zamani sana? Hivyo, watu hunichukia kila mara kwa ajili ya kero lote ambalo kuweko Kwangu huwasababishia. Kama Nisingekuwepo, wangeweza kufurahia baraka za ufalme wakati wa sasa—na kungekuwa na haja gani kuvumilia mateso

haya? Na kwa hiyo Nawaambiwa watu ni heri wangeondoka, kwamba wanapaswa kujinufaisha na jinsi mambo yanavyoendelea vizuri wakati huu ili kujitafutia njia ya kutoka; wanahitaji kujinufaisha na wakati huu, huku wakiwa bado wachanga, kujifunza ujuzi fulani. Wasipofanya hivyo, katika siku za baadaye watakuwa wamechelewa sana. Katika nyumba Yangu, hakuna ambaye amewahi kupokea baraka. Mimi huwaambia watu waharakishe kuondoka, wasishikilie kuishi katika “umaskini”; katika siku za baadaye watakuwa wamechelewa sana kujuta. Msijilaumu sana: mbona ujisumbue? Hata hivyo Mimi pia huwaambia watu kwamba wanapokosa kupata baraka, mtu yeyote asilalamike kunihusu. Sina wakati wa kupotezea maneno Yangu kwa mwanadamu. Natumaini kwamba watu watakumbuka jambo hili, kwamba wasilisahau—maneno haya ni ukweli usio na raha kutoka Kwangu. Nilipoteza imani kwa mwanadamu kitambo sana, Nilipoteza tumaini kwa watu kitambo sana, kwani wanakosa lengo, hawajawahi kuweza kunipa moyo unaompenda Mungu, na wao kila mara hunipa misukumo yao badala yake. Nimesema mengi kwa mwanadamu, na kwa kuwa bado watu wanapuuza ushauri Wangu leo, Mimi huwaambia kuhusu maoni Yangu ili kuwazuia kuuelewa vibaya moyo Wangu katika siku za baadaye; kama wataishi au kufa katika nyakati zijazo ni shauri yao, Sina mamlaka juu ya jambo hili. Natumaini watapata njia yao wenyewe ya kuendelea kuishi, nami Sina mamlaka katika hili. Kwa sababu mwanadamu hanipendi kwa kweli, tunatengana tu; katika siku za baadaye, hakutakuwa tena na maneno yoyote kati yetu, hatutakuwa tena na jambo la kuzungumzia, hatutaingiliana, kila mmoja wetu atashika njia yake, watu wasije kunitafuta, Sitawahi tena kutaka msaada kutoka kwa mwanadamu. Hili ni jambo linalotuhusu sisi, na tumezungumza bila kuwapotosha watu ili kuzuia kuweko kwa masuala yoyote katika siku za baadaye. Je, hili haliyafanyi mambo kuwa rahisi zaidi? Kila mmoja wetu aende njia yake na tusiwe na uhusiano wowote kati yetu—hilo lina kosa gani? Natumaini watu watalifikiria hili.

Mei 28, 1992

Sura ya 47

Ili kuwafanya wanadamu wawe wakomavu katika maisha na kuwafanya wanadamu na Mimi tuweze kutimiza matokeo katika udhanifu wetu wa pamoja, Nimewaendeka wanadamu kila mara, Nikiwakubalia kupata chakula na riziki kutoka kwa neno Langu na kupokea utele Wangu kutoka kwake. Sijawahi kuwapa wanadamu sababu ya kuaibika, lakini mwanadamu hafikirii hisia Zangu kamwe. Hii ni kwa sababu wanadamu hawana hisia na “hudharau” vitu vyote isipokuwa Mimi. Kutokana na dosari za wanadamu, Nawasikitikia sana na hivyo Nimefanya kila Niwezalo, ili waweze kufurahia utele wa dunia hadi kiasi cha kuiridhisha mioyo yao kwa wakati wao duniani. Simtendei mwanadamu bila haki na kwa kuzingatia watu walionifuata kwa miaka mingi, Nimekuwa na moyo wa huruma kwao. Ni kama kwamba Siwezi

kujizuia kuweka mikono Yangu juu yao ili kufanya kazi Yangu. Kwa hiyo, Nawaangalia watu waliokonda wanaonipenda jinsi wanavyojipenda wenyewe na katika moyo Wangu daima huwa kuna hisia za maumivu zisizoweza kuelezeka, lakini ni nani angevunja mkataba kwa sababu ya hili? Ni nani angesumbua kwa sababu ya hili? Hata hivyo, Nimewakirimu wanadamu zawadi Zangu zote ili waweze kuzifurahia kwa ukamilifu, nami Sijawatesa wanadamu kuhusu suala hili. Ndio maana wanadamu bado wanauona uso Wangu wa huruma na wenye ukarimu. Nimevumilia na kusubiri kila mara. Wakati ambapo wanadamu wanafurahia kwa kuridhika na kisha kuchoshwa, Nitaanza “kukidhi” maombi yao na kuwaruhusu wanadamu wote kuepuka maisha yao matupu, na kisha Sitakuwa na shughuli tena na watu. Juu ya dunia, hapo awali Nilikuwa Nimewameza binadamu na maji ya bahari, Nilikuwa Nimewadhibiti kwa njaa, Nilikuwa Nimewatisha kwa tauni za wadudu, na Nilikuwa Nimetumia mvua nzito “kuwanyunyizia”, lakini mwanadamu hakuhisi utupu wa maisha hata kidogo. Sasa bado mwanadamu haelewi umuhimu wa kuishi duniani. Yawezekana kuwa kuishi katika kuwepo Kwangu ni kipengele muhimu sana cha maisha ya binadamu? Je, kuishi ndani Yangu kunamruhusu mtu kuepuka tishio la maafa? Ni miili mingapi ya nyama duniani imeishi katika uhuru wa kujifurahisha? Ni nani ameeepuka utupu wa kuishi katika mwili? Na nani angeujua? Tangu uumbaji Wangu wa wanadamu hadi sasa, hakuna ambaye ameishi maisha muhimu sana duniani, na hivyo mwanadamu daima amekuwa mzembe kwa kuishi maisha yasiyo na umuhimu kabisa, lakini hakuna yeyote aliye na nia ya kuepuka mashaka haya na hakuna yeyote aliye na nia ya kuepukana na maisha yake matupu na ya uchovu. Katika uzoefu wa wanadamu, hakuna hata mmoja wa wale wanaoishi katika mwili ameeepukana na desturi za ulimwengu wa mwanadamu, hata ingawa wanaitumia kwa faida ya kunifurahia Mimi. Badala yake, daima wameruhusu tu asili ifuate mkondo wake na kujidanganya.

Wakati Nitakapomaliza kabisa kuwepo kwa wanadamu, hakutakuwa na mtu aliyeachwa kuvumilia mateso kutoka duniani, na kisha kazi Yangu kuu inaweza kusemwa kuwa imetimizwa kwa ukamilifu. Katika siku za mwisho wakati Mimi Nimefanyika mwili, kile Ninachotaka kukamilisha katika kazi Yangu ni kuwawezesha wanadamu kuelewa utupu wa kuishi katika umbo la mwili, na hivyo Nitauzima mwili. Baadaye, hakutakuwa na watu duniani, hakuna mtu atakayelia tena kuhusu utupu wa dunia, hakuna mtu atakayeongea tena juu ya matatizo ya mwili, hakuna mtu atakayelalamika tena kuwa mimi Sifanyi haki, na watu na vitu vyote vitaingia katika pumziko. Baadaye, hakuna mtu atakayekuwa akirupuka, wala kutafuta hapa na pale duniani kwa sababu watu watakuwa wamejipatia hatima ya kufaa. Wakati huo, watakuwa na tabasamu kwenye nyuso zao. Halafu Sitamwuliza mwanadamu chochote tena na Sitakuwa na mgogoro zaidi naye; hapatakuwa na mkataba wa amani tena kati yetu. Naishi juu ya dunia na wanadamu wanaishi juu ya dunia; Naishi na kukaa pamoja nao. Wanadamu wanahisi furaha ya kuwepo

Kwangu; kwa hivyo wanadamu hawako radhi kuondoka bila sababu, na badala yake, wangependelea kuwa Nikae tu kwa muda kidogo zaidi. Ningewezaje kuvumilia kuona matukio ya taabu yaliyoenea ulimwenguni huku Nikose kujitahidi hata kidogo ili kusaidia? Mimi si wa dunia. Ni kupitia uvumilivu ndio Nabaki duniani hadi siku hii, ingawa Nafanya hivyo kwa kusita. Isingalikuwa kwa ajili ya kuomba kwa wanadamu kusio na mwisho, Ningeliondoka zamani. Siku hizi wanadamu wanaweza kujitunza na hawahitaji msaada Wangu kwa sababu wamekomaa nao hawahitaji Niwalishe. Kwa hiyo Napanga kufanya sherehe ya ushindi na wanadamu, baada ya hapo Nitawaaga, ili waweze kujua jambo hili. Bila shaka, kutengana tukiwa tumekosana halingekuwa jambo jema kwa sababu hakuna machukio kati yetu. Kwa hivyo urafiki ulioko kati yetu utakuwa wa milele. Natumaini kwamba baada ya sisi kutengana, wanadamu wanaweza kutekeleza “urithi” Wangu na kutosahau kuhusu mafundisho ambayo Nimetoa wakati wa maisha Yangu, kutofanya lolote ambalo lingelea aibu kwa jina Langu, na kukumbuka neno Langu. Natumaini kwamba binadamu watajitahidi kabisa kuniridhisha Mimi Nitakapokuwa Nimeondoka. Natumaini kuwa binadamu watatumia neno Langu kama msingi wa maisha yao. Msinivunje moyo kwa sababu moyo Wangu daima umekuwa ukiwajali wanadamu na Mimi Nimewapenda daima. Binadamu na Mimi tulikusanyika pamoja wakati mmoja na kufurahia duniani baraka hizo hizo zilizo mbinguni. Niliishi pamoja na wanadamu na kukaa pamoja nao, wanadamu walinipenda daima, nami Niliwapenda daima; tulikuwa na uhusiano kati yetu. Ninapokumbuka wakati Wangu pamoja na wanadamu, Nakumbuka siku zetu zikijawa na kicheko na furaha, na zaidi ya hayo, kulikuwa na ugomvi. Hata hivyo, upendo kati yetu uliimarishwa kwa msingi huu na kushughulikiana kwetu hakukuwahi kuvunjika. Kati ya miaka yetu mingi ya mawasiliano, wanadamu wameacha alama kubwa juu Yangu nami Nimewapa wanadamu mambo mengi ili wafurahie, ambayo wanadamu daima wameonyesha shukrani kubwa kuyahusu. Sasa, mkutano wetu ni tofauti na kitu chochote cha awali; nani angeweza kukosa wakati huu wa kuagana kwetu? Wanadamu wananipenda sana, nami Nina upendo usio na mwisho kwao, lakini ni nini kinaweza kufanywa kuhusu hilo? Nani angethubutu kwenda kinyume na mahitaji ya Baba wa mbinguni? Nitarejea kwenye makao Yangu, ambapo Nitakamilisha sehemu nyingine ya kazi Yangu. Pengine tutapata nafasi ya kukutana tena. Ni matumaini yangu kuwa wanadamu hawatahisi huzuni sana na kwamba wataniridhisha Mimi duniani; mara nyingi Roho Wangu aliye mbinguni Atawapa neema.

Katika wakati wa uumbaji, Nilikuwa nimetabiri kwamba katika siku za mwisho Nitafanya kundi la watu ambao wana nia moja na Mimi. Nilikuwa nimetabiri kwamba baada ya kuanzisha mfano duniani katika siku za mwisho, Nitarudi kwenye makao Yangu. Wakati wanadamu wote wameniridhisha Mimi, watakuwa wametimiza matakwa Yangu, na Mimi Sitahitaji tena kitu chochote kutoka kwao. Badala yake, wanadamu na Mimi tutasimuliana hadithi za siku zetu za

zamani na baada ya hapo tutaagana. Naanza kuifanya kazi hii na kuwawezesha wanadamu kujiandaa kiakili. Nitawawezesha wanadamu wote kuelewa nia Zangu ili wasinieleme vibaya au kufikiria kuwa Mimi ni katili au asiye na huruma, ambayo sio nia Yangu. Je, wanadamu wananipenda lakini wanakataa kuniacha Niwe na mahali pa kupumzika pa kufaa? Je, wanadamu hawataki kumsihi Baba wa mbinguni kwa ajili yangu? Je, wanadamu hawajalia machozi ya huruma pamoja na Mimi? Je, wanadamu hawajasaidia katika kufanikisha mkutano wa haraka wa Sisi Baba na Mwana? Kwa nini hawataki sasa? Huduma Yangu duniani imetimizwa na baada ya kuagana na wanadamu bado Nitaendelea kuwasaidia wanadamu, je, hivi si vizuri? Ili kazi Yangu ipate kuwa na ufanisi zaidi na ili iwe ya manufaa pande zote, lazima tuagane ingawa ni uchungu kufanya hivyo. Machozi yetu yatatiririka kimyakimya na Sitawashutumu wanadamu tena. Katika wakati uliopita, Nilisema mambo mengi ambayo yaliichoma moyo halisi wa wanadamu, yakiwasababisha kutoa machozi ya huzuni. Kwa hiyo, Naomba radhi kwa wanadamu na kuomba msamaha wa wanadamu; msinionee kijicho na kunichukia, kwa kuwa haya yote ni kwa ajili ya manufaa yao wenyewe. Kwa hiyo, Natumaini kwamba wanadamu watauelewa moyo wangu. Katika nyakati za awali, tulikuwa na migogoro yetu, lakini tukiangalia nyuma, sisi sote tulifaidika. Kupitia kwa migogoro hii Mungu na wanadamu wamekuza daraja la urafiki kati yao, je, hili si tunda la jitihada zetu za ushirikiano? Sote tunapaswa kufurahia hili. Namwomba mwanadamu anisamehe kwa “makosa” Yangu ya awali na dhambi za wanadamu pia zitasahauliwa. Maadamu mwanadamu anaweza kurudisha upendo Wangu katika siku zijazo, basi hilo litaifariji Roho Yangu mbinguni. Sijui ni nini azimio la wanadamu katika suala hili, au kama mwanadamu ana nia ya kutimiza ombi Langu la mwisho au la. Siombi chochote kingine kutoka kwa wanadamu, ila tu wanipende na hiyo inatosha. Je, hili linaweza kufanywa? Yaache mambo yote mabaya yaliyotokea kati yetu yawe katika wakati uliopita, acha kuwe na upendo kati yetu daima. Nimewapa wanadamu upendo mwingi sana na wanadamu wamelipa gharama kubwa sana kwa ajili ya kunipenda Mimi. Hivyo, Natumaini kwamba binadamu watathamini upendo safi na takatifu kati yetu ili upendo wetu uenee kote katika dunia ya wanadamu na kupitishwa kwa vizazi vingine milele. Tutakapokutana tena, hebu tuungane katika upendo ili upendo wetu uweze kuendelea milele na kusifiwa na kuzungumziwa na watu wote. Hili lingeniridhisha na Ningewaonyesha wanadamu uso Wangu wenye tabasamu. Natumaini kwamba wanadamu watakumbuka yote Niliyowakabidhi.

Juni 1, 1992

Kiambatisho:
Ufafanuzi wa Mafumbo ya Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu
Mzima

(Ufafanuzi wa Baadhi ya Sura)

Sura ya 1

Kama tu Mungu alivyosema, “Hakuna anayeweza kuelewa mzizi wa maneno Yangu au kusudi la maneno haya.” Kama Isingekuwa uongozi wa Roho wa Mungu, kama isingekuwa kwa majilio ya maneno Yake, wote wangeangamia chini ya kuadibu Kwake. Ni kwa nini Mungu humjaribu mwanadamu kwa muda mrefu hivyo? Na kwa muda mrefu kama miezi mitano? Hili ndilo wazo la kulenga la ushirika wetu na vilevile wazo kuu katika hekima ya Mungu. Tunaweza kuchukulia kwamba: Isingekuwa jaribio hili, na bila Mungu kushambulia, kuua, na kuwatema binadamu wapotovu, ikiwa ujenzi wa kanisa ungeendelea mpaka leo, basi hilo lingefanikisha nini? Kwa hiyo katika mstari wa kwanza wa hotuba Yake, Mungu anaenda moja kwa moja kwa wazo hilo na kueleza athari inayotakiwa ya kazi ya miezi hii, na ni sahihi kabisa! Inaelekea kuonyesha hekima ya matendo ya Mungu katika kipindi hiki cha wakati: kuwafunza watu kujifunza utii na kujitolea kwa uaminifu kupitia majaribio, na vilevile jinsi ya kumfahamu Mungu bora kupitia usafishaji wa uchungu. Kadri watu wanavyopitia kukata tamaa, ndivyo wanavyoweza kujifahamu wenyewe. Na kusema kweli, kadri wanavyopitia usafishaji wa uchungu, ndivyo wanavyoweza kufahamu zaidi upotovu wao wenyewe, na kwa kufanya hivyo hata wanajifunza kwamba hawastahili kuwa mtendaji huduma wa Mungu, na kufanya aina hii ya huduma ni kuinuliwa na Yeye. Na kwa hiyo mara tu hili linapotimizwa, mara tu mwanadamu anapojipunguza mwenyewe, Mungu hutamka maneno ya huruma, bila kufichwa chochote. Tayari inaweza kuonekana wazi kwamba njia za utendakazi wa Mungu, baada ya muda wa miezi hii michache, inazingatia leo kama mwanzo wa kazi ya Mungu, Ameifanya hii bayana kwa wote kuona. Katika wakati uliopita, Mungu alisema mara kwa mara “si rahisi kustahili haki ya kuitwa watu Wangu,” kwa hiyo kama Alivyotimiza maneno haya ndani ya watu wanaotajwa kama watendaji huduma, wote huenda wakaona kwamba Mungu anaweza kuaminiwa bila kosa lolote. Yote ambayo Mungu husema yatakuwa kweli kwa viwango tofautitofauti, na maneno Yake sio matupu hata kidogo.

Wanadamu wote wanapokuwa wenye kuhangaika na wa kusikitishwa, maneno haya kutoka kwa Mungu huwa na maana kwa wote wanaojikuta hawana matumaini, na huwahuisha wao. Ili kuondoa shaka zaidi, Mungu aliongeza kwamba “ingawa wanatajwa kama watu Wangu, jina hili si la chini ya kuitwa ‘wana’ Wangu.” Hapa mtu anaweza kuona kwamba Mungu pekee ndiye anaweza kuhifadhi mamlaka Yake, na watu wakishayasoma wanaamini thabiti zaidi kwamba hii sio njia ya kufanya kazi, bali ukweli. Tukisonga hatua moja zaidi, ili maono ya watu yasiwe yenye kufunikwa na giza, utambulisho wa kila mtu unafanywa bayana. Hili ni toshelezi kuonyesha hekima ya Mungu. Hivi watu wanaweza kufahamu bora kwamba Mungu anaweza

kuona ndani kabisa ya mioyo ya wanadamu; kama vile makaragosi, yote wanayofanya na yote wanayofikiria yanaendeshwa na Mungu. Hili ni thabiti.

Tukirudi mwanzo, kile Mungu alisema kwanza ni kwamba hatua ya kwanza ya kazi Yake, “kulitakasa kanisa,” ishakamilishwa. “Hali sio kama ilivyokuwa wakati fulani, na kazi Yangu imeingia katika kiwango kipa cha kwanza.” Kutokana na kauli hii, mtu anaweza kuona kwamba kazi ya Mungu imeingia katika kiwango kipa cha kwanza, na punde baada ya Yeye kutaja mpango makini wa hatua inayofuata ya kazi Yake kwetu—baada ya kumaliza ujenzi wa kanisa, maisha ya Enzi ya Ufalme yataanza. “Kwani sasa sio enzi ya kujenga kanisa tena, lakini badala yake ni enzi ambamo ufalme unajengwa kwa ufanisi.” Kuongezea, Ameonyesha kwamba kwa vile watu bado wako duniani, makusanyiko yao yataendelea kutajwa kama kanisa, kwa njia hii kusaidia kuepuka utambuzi usio wa kweli wa ufalme jinsi kila mtu amefikiria kuwa. Kinachofuata, Nitakuwa na ushirika juu ya suala la maono.

Sasa ni enzi ya ujenzi wa ufalme na mwisho wa ujenzi wa kanisa; ilhali, ni kwa nini makusanyiko yote bado yataitwa kanisa? Imetajwa hapo awali kwamba kanisa ni utangulizi wa ufalme; bila kanisa hakungekuwa na mazungumzo kuhusu ufalme. Enzi ya Ufalme inaanza na Mungu akitekeleza huduma Yake katika mwili, na Enzi ya Ufalme inaletwa na Mungu mwenye mwili. Anacholeta ni Enzi ya Ufalme, sio majilio rasmi ya ufalme. Hili si gumu kuwaza; watu wanaozungumziwa ni watu wa Enzi ya Ufalme, sio watu wa ufalme wenyewe. Hivyo, inaeleweka kwamba makusanyiko duniani bado yangetajwa kama kanisa. Hapo zamani, Alitenda kupitia kwa ubinadamu Wake wa kawaida, na hakushuhudiwa kama Mungu Mwenyewe, hivyo Enzi ya Ufalme haikuwa imeanza miongoni mwa wanadamu; yaani, kama Nilivyosema, Roho Wangu hakuwa ameanza kufanya kazi rasmi ndani ya umbo Langu lenye mwili. Kwa vile sasa Mungu Mwenyewe ameshuhudiwa, ufalme umetambuliwa miongoni mwa wanadamu. Hili linaashiria kwamba Nitaanza kufanya kazi kupitia kwa uungu, na hivyo wale wanaoweza kukubali maneno Yangu na matendo Yangu katika uungu wanajulikana kama watu Wangu wa Enzi ya Ufalme. Ni kutokana na haya ambapo neno “watu Wangu” liliibuka. Katika hatua hii, kimsingi Nafanya kazi na kuzungumza kupitia kwa uungu Wangu. Mwanadamu hawezi kuingilia, wala kuweza kuvuruga mpango Wangu. Mara tu neno la Mungu lifikapo kiwango fulani, jina Lake hushuhudiwa, na majaribio Yake ya wanadamu huanza. Hiki ndicho kilele cha hekima katika kazi ya Mungu. Hiki kinaweka msingi imara na kukita mizizi kwa ajili ya kuanza hatua inayofuata na vilevile hitimisho la hatua ya mwisho. Mwanadamu hakuwa na njia ya kulijua hilo; hiki ndicho kiwango cha kukutana cha sehemu ya kwanza na ya pili ya enzi ya hukumu. Bila miezi michache ya usafishaji wa mwanadamu, Sikuweza kufanya kazi kupitia uungu Wangu. Hii miezi ya usafishaji hufungua njia ya hatua inayofuata ya kazi Yangu. Mwisho wa kazi hii ya miezi michache ni ishara ya kuingia ndani zaidi katika awamu inayofuata ya kazi.

Ikiwa mtu kweli anaelewa maneno ya Mungu, mtu huenda akaelewa kwamba Anatumia miezi hii kuanza hatua inayofuata ya kazi Yake ili iweze kuzaa matunda zaidi. Kipingamizi cha binadamu Wangu kimesababisha kizuizi kwa ngazi inayofuata ya kazi Yangu, kwa hiyo kupitia hii miezi ya usafishaji wa uchungu, pande zote mbili zinaadilishwa na kupata ubora kamili. Ni hivi sasa tu, kutokana na hii ndipo mwanadamu anaanza kuthamini njia Yangu ya kumrejelea. Kwa hiyo, wakati Mungu kwa kueleza kalamu Yake, alisema Hatamwita tena mwanadamu “mtendaji-huduma,” lakini badala yake “watu Wake,” wote walijawa na furaha. Ilikuwa hasa kwa sababu ya kushikilia unyonge wa mwanadamu ndiyo Mungu aliyozungumza jinsi Alivyozungumza.

Ili kuwaridhisha zaidi wanadamu wote na kuonyesha najisi ndani ya ibada ya watu wengine, Mungu ameenda mbele zaidi kuonyesha sehemu mbalimbali zisizovutia za wanadamu, na kwa njia hii Ametimiza maneno Yake kama yafuatayo: “Ni wangapi wanapenda Mimi kweli? Ni nani asiyetenda kwa kuzingatia siku zake mwenyewe za baadaye? Ni nani hajawahi kulalamika wakati wa majaribio yake?” Kutokana na maneno haya, wanadamu wanaweza kuona kutotii kwao wenyewe, kutokuwa waaminifu na ukosefu wa utiifu kwa mzazi, na hivyo kuona huruma na upendo wa Mungu vikiwafuata wote wanaomtafuta Yeye katika kila hatua ya njia. Hili linaweza kuonekana kutokana na maneno haya: “Sehemu ya mwanadamu inapokuwa karibu kabisa kurudi nyuma, wakati wote wanaonitarajia Mimi kubadilisha mtindo Wangu wa kuhutubu wanakosa tumaini, Ninatamka maneno ya wokovu, na kuwarudisha wote wanipendao Mimi kweli kwa ufalme Wangu, mbele ya kiti Changu cha enzi.” Hapa, kirai “wale wanipendao Mimi kweli,” na swali la balagha “Ni wangapi wanipendao Mimi kweli?” havipingani. Inaonyesha kwamba wale ambao ni wa kweli wana najisi. Sio kama kuwa Mungu hajui chochote. Kwa vile Mungu anaweza kuona sehemu ya ndani zaidi ya mioyo ya wanadamu, neno “kweli” linatumiwa kwa stihizai kwa kurejelea upotovu wa wanadamu, ili wanadamu wote waweze kuona vizuri kuwa kwao wadeni wa Mungu, wachukue lawama zaidi, na vilevile kutambua ukweli kwamba malalamiko yaliyo ndani ya mioyo yao yote yanatoka kwa Shetani. Kila mtu anashangaa anapooa neno kama “ibada,” akifikiri kwa ndani: “Mara nyingi mimi nimekosoa Mbingu na dunia, na mara nyingi nimetaka kuondoka, lakini kwa vile niliogopa amri za usimamizi za Mungu nilivumilia tu na kushirikiana na umati, kumngoja Mungu anishughulikie, nikifikiria kwamba iwapo mambo yangetokea kuwa yasiyo na matumaini kweli, bado kungekuwa na muda wa kutosha wa kujiondoa polepole. Lakini sasa Mungu anaituita sisi watu Wake waliojitolea, kwa hiyo hii inamaanisha kwamba Mungu kwa kweli anaweza kuona moja kwa moja ndani ya sehemu ya ndani kabisa ya mioyo ya wanadamu?” Ni mpaka mwisho kabisa ndipo Mungu alionyesha hali za ndani za aina mbalimbali ya watu ili kuepuka aina hii ya suitafahamu. Hili liliwafanya wanadamu ambao hapo mwanzo walikuwa wenye shaka ndani ya mioyo yao lakini

wenye furaha katika maneno yao kuingia katika hali ya kuondoa shaka ndani ya moyo, maneno, na macho. Kwa njia hii, fikira za mwanadamu za maneno ya Mungu zimekuwa kubwa zaidi, na kulingana na hilo mwanadamu amekuwa na woga zaidi, uchaji zaidi, na amepata ufahamu bora zaidi wa Mungu. Hatimaye, ili kupunguza wasiwasi wa mwanadamu, Mungu alisema: “Lakini kwa vile siku zilizopita ni siku zilizopita, na sasa ni wakati uliopo, hakuna haja ya kutamani tena siku zilizopita, au kuwa na wasiwasi kuhusu siku za usoni.” Aina hii ya njia ya kuzungumza ya haraka, patanifu, ilhali ya mkato ina hata athari kubwa zaidi, ikiwaruhusu wote wanaoyasoma maneno Yake kuiona nuru mara nyingine katika kufa moyo kwao, halafu waone hekima na matendo ya Mungu, kisha wapate jina la heshima la “watu wa Mungu,” na baada ya hapo waondoe shaka iliyo ndani ya moyo yao, na kisha waje kujijua wao wenyewe kutokana na miundo ya mabadiliko ya hali zao mbalimbali za akilini. Hali hizi huonekana katika zamu, simanzi pamoja na huzuni, na furaha na shangwe. Mungu ameteka muhtasari wa mfano wa maisha wa watu katika sura hii. Ni dhahiri kwa kiwango cha ukamilifu, kitu ambacho mwanadamu havezi kutimiza. Inafichua kwa kweli siri zilizo ndani kabisa ya moyo wa mwanadamu. Je, hili ni jambo ambalo mwanadamu angefanya?

Hata muhimu zaidi ni fungu la maneno lililo hapa chini, ambamo Mungu anafichua kwa mwanadamu moja kwa moja amri Yake ya usimamizi. Na hii ndiyo sehemu muhimu zaidi: “Miongoni mwa wanadamu, wale wanaoenda kinyume cha uhalisi na hawafanyi mambo kulingana na uongozi Wangu hawatakuwa na mwisho mzuri, na watajiletea tu matatizo. Kwa kila kitu kinachotokea ulimwenguni, hakuna kitu Nisichokuwa na usemi wa mwisho kukihusu.” Je, hii sio amri ya usimamizi ya Mungu? Inaelekea kuonyesha kwamba kuna mifano mingi ya wale ambao hutenda dhidi ya amri hii ya usimamizi. Zaidi ya hayo, inamwonya kila mtu asifikirie juu ya kudura yake mwenyewe. Ikiwa mtu anataka kuutoroka mpango wa Mungu, matokeo yatakuwa ya kutisha yapitayo mawazo. Hivyo, inawafanya wale wote wanaopitia kupata nuru na mwangaza katika maneno haya waweze kuelewa bora zaidi amri ya usimamizi ya Mungu na vilevile kuelewa kwamba uadhama Wake usikosewe, na hivyo kuwa wenye uzoefu zaidi na watulivu na waliomakinika, wa kijani kibichi kama msonobari uliopona ambao umekiuka vitisho vya baridi kali, unaoendelea kuongeza kwa uzima wa kijani kibichi kinachostawi cha asili. Kauli hii huwafanya watu wengi wahisi kukanganyikiwa kisulisuli, kana kwamba wamepotelea katika aina fulani ya mzingile; hili ni kwa sababu maudhui ya maneno ya Mungu hubadilika upesi kiasi, kwa hiyo watu tisa kutoka kwa kumi huingia katika matata mengi wanapojaribu kufahamu tabia zao wenyewe za upotovu. Kwa ajili ya kufanya kazi kwa urahisi, kuondoa shaka ya mwanadamu, na ili wote waweze kuamini zaidi katika uaminifu wa Mungu, Anasisitiza mwisho wa kifungu hicho cha maneno: “kila mmoja wa wale wanaonipenda kweli watarudi mbele ya kiti Changu cha enzi.” Hivyo, wale wote ambao wamepitia miezi mingi ya

kazi Yake wanapunguziwa huzuni yao mara moja; mioyo yao, ambayo ilihisi kana kwamba imening'inizwa katikati ya hewa, hurudi kwa hali yao ya awali kana kwamba jiwe limeangushwa kwa ardhi ngumu. Wao hawana tena haja ya kufikiria kuhusu majaliwa yao; aidha, wanaamini kwamba Mungu atazungumza maneno matupu tena. Kwa vile wanadamu ni wa kujidai, hakuna hata mmoja asiyeamini kwamba anaonyesha kujitolea kwa juu sana kwa Mungu; hii ndiyo maana kwa makusudi Mungu anasisitiza “kweli”—ni kutimiza matokeo makuu zaidi. Hii ni njia na kuweka msingi wa hatua inayofuata katika kazi Yake.

Sura ya 3

Leo si tena Enzi ya Neema, wala enzi ya rehema, bali ni Enzi ya Ufalme ambamo watu wa Mungu wanafichuliwa, enzi ambayo kwayo Mungu hufanya mambo moja kwa moja kwa njia ya uungu. Hivyo, katika sura hii cha maneno ya Mungu, Mungu huongoza wale wote ambao wanayakubali maneno Yake katika ulimwengu wa kiroho. Katika aya ya ufunguzi, Anatangulia kufanya maandalizi haya, na ikiwa mtu ana maarifa ya maneno ya Mungu, atafuata nyuki ili apate asali, na ataelewa moja kwa moja kile ambacho Mungu Anatamani kutimiza kwa watu Wake. Hapo kabla, watu walikuwa wanapimwa kupitia cheo cha “wafanya huduma,” na leo, baada ya wao kuathiriwa na majaribu, mafunzo yao huanza rasmi. Aidha, watu lazima wawe na ufahamu mkubwa juu ya kazi ya Mungu katika msingi wa maneno ya wakati uliopita, na wanapaswa kuyaangalia maneno na mtu, na Roho na mtu, kama kitu kimoja kamili kisichoachana—kama kinywa kimoja, moyo mmoja, tendo moja, na chanzo kimoja. Matakwa haya ni matakwa ya kiwango cha juu sana ambayo Mungu Ameyafanya kwa mwanadamu tokea uumbaji. Kutoka kwa hili inaweza kuonekana kwamba Mungu anatamani kutumia sehemu ya jitihada Zake kwa watu Wake, kwamba Anatamani kuonyesha ishara na maajabu kadhaa ndani yao, na, muhimu zaidi, kwamba Anatamani kuwafanya watu wote kutii kazi na maneno yote ya Mungu kikamilifu. Kwa upande mmoja, Mungu Mwenyewe Anashikilia ushuhuda Wake, na kwa upande mwingine, Ameweka matakwa kwa watu Wake, na moja kwa moja Ametoa kwa umma amri ya Mungu ya kiusimamizi: Hivyo, kwa kuwa mnaitwa watu Wangu, mambo hayapo kama yalivyokuwa; mnapaswa kusikiliza na kutii matamshi ya Roho Wangu, fuateni kwa karibu kazi Yangu, na msitenganishe Roho Wangu na mwili Wangu, maana kwa asili Sisi ni wamoja, na Hatujatengana. Katika hili, ili kuwazuia watu wasimpuuze Mungu mwenye mwili, mara nyingine tena msisitizo unawekwa kwa “maana kwa asili Sisi ni wamoja, na Hatujatengana”; kwa sababu kupuuzia huko ni kuanguka kwa mwanadamu, hii kwa mara nyingine tena imeorodheshwa katika amri za Mungu za kiusimamizi. Kisha, Mungu huwataarifu watu juu ya athari za kukosea amri za Mungu za kiusimamizi, bila kuficha kitu chochote, kwa kusema “watapata hasara, na wataweza tu kunywa kutoka kwenye kikombe chao chungu.” Kwa sababu mwanadamu ni dhaifu, baada ya kuyasikia maneno haya hana budi ila kuwa macho dhidi ya

Mungu moyoni mwake maana “kikombe chungu” kinasosha kuwafanya watu watafakari kwa muda. Watu wana tafsiri nyingi za hiki “kikombe chungu” ambapo Mungu Anazungumza: kuhukumiwa na maneno au kufukuzwa kutoka katika ufalme, au kutengwa kwa muda fulani, au mwili wa mtu kuharibiwa na Shetani na kuingiwa na pepo wabaya, au kutelekezwa na Roho wa Mungu, au mwili wa mtu kukomeshwa na kupelekwa Kuzimu. Tafsiri hizi ndizo akili za watu zinaweza kutimizwa, na hivyo katika mawazo yao, watu hawawezi kuzizidi. Lakini mawazo ya Mungu si kama ya mwanadamu; ni sawa na kusema “kikombe chungu” hakirejelei chochote kati ya hayo hapo juu, bali ni kwa kiwango cha ufahamu wa watu juu ya Mungu baada ya kushughulikiwa na Mungu. Kulifanya hili lieleweke vizuri zaidi, mtu anapotenga kiholela Roho wa Mungu na maneno Yake, au anatenganisha maneno na mtu, au Roho na mwili ambao Yeye Mwenyewe huuvaa, mtu huyu si kwamba hawezi tu kumjua Mungu katika maneno ya Mungu, lakini pia anapokuwa na shaka kidogo na Mungu—atakuwa na upofu mara kwa mara. Si kama watu wanavyodhani kwamba wameondolewa moja kwa moja; badala yake, pole pole wanaanguka katika adabu ya Mungu—ambayo ni sawa na kusema, wanatumbukia kwenye janga kubwa sana, na hakuna anayeweza kulingana nao, kana kwamba wameingiwa na pepo wabaya, na kana kwamba wao ni nzi wasiokuwa na kichwa, wakigonga vitu kila wanapokwenda. Licha ya hili, bado hawawezi kuondoka. Katika mioyo yao, mambo ni magumu kiasi kisichoelezeka, kana kwamba kuna mateso yasiyoelezeka moyoni mwao—lakini hawawezi kufungua vinywa vyao, na wanashinda siku nzima wakiwa wamezubaa, wakiwa hawawezi kumhisi Mungu. Ni katika mazingira haya ndipo amri za Mungu za kiusimamizi zinawatisha, kiasi kwamba hawawezi kuliacha kanisa licha ya kutokuwa na furaha—hiki ndicho kile kinachoitwa “mashambulizi ya ndani na ya nje,” na ni vigumu sana watu kuvumilia. Kile kilichosemwa hapa ni tofauti na dhana za watu—na hiyo ni kwa sababu, kwa hali ilivyo, bado wanajua kumtafuta Mungu, na hii hutokea pale ambapo Mungu Anawakwepa, na kitu ambacho ni muhimu zaidi ni kwamba, kama tu mtu asiye muumini, hawawezi kabisa kumhisi Mungu. Mungu hawaokoi moja kwa moja watu kama hao; wakati vikombe vyao chungu vitakapomwagika, hapo ndipo wakati ambapo siku yao ya mwisho itakuwa imewasili. Lakini kwa wakati huu, bado wanatafuta mapenzi ya Mungu, wakitamani kufurahi zaidi kidogo tu—lakini wakati huu ni tofauti na zamani, isipokuwa kama kuna hali mahususi.

Kufuatia hili, Mungu pia Anaelezea kipengele chema kwa wote na hivyo kwa mara nyingine tena wanapata maisha—kwa kuwa, katika nyakati za zamani, Mungu alisema kwamba wafanya huduma hawakuwa na maisha, lakini leo kwa ghafula Mungu huzungumzia juu ya “maisha yaliyomo ndani.” Ni kwa mazungumzo tu ya maisha ndipo watu wanajua kwamba bado kunaweza kuwa na maisha ya Mungu ndani yao. Kwa namna hii, upendo wao kwa Mungu huongezeka mara kadhaa, na wanapata maarifa makubwa zaidi ya upendo na rehema ya Mungu.

Hivyo, baada ya kuyaangalia maneno haya, watu wote hutubu makosa yao ya nyuma, na kwa siri wanatokwa na machozi ya toba. Wengi pia, kimyakimya wanaamua kwamba ni lazima wamridhishe Mungu. Wakati mwingine, maneno ya Mungu yanachoma ndani kabisa kwenye mioyo ya watu, na kufanya kuwa vigumu kwa watu kuyakubali, na vigumu kwa watu kuwa na amani. Wakati mwingine, maneno ya Mungu ni ya kweli na ya dhati, na huwafurahisha watu, kiasi kwamba baada ya watu kuwa wameyasoma, ni kama wakati ambapo mwanakondoo anamwona mama yake baada ya miaka mingi ya kupotea. Machozi yanajaa machoni mwao, wanaelemewa na hisia, na wana shauku ya kujirusha kwenye kumbatio la Mungu, wakiwa wamejawa na kikweukweu, wakiondoa maumivu yasiyoelezeka ambayo yamekuwa mioyoni mwao kwa miaka mingi ili kuonyesha utiifu wao kwa Mungu. Kwa sababu ya majaribio ya miezi kadhaa, wamekuwa wepesi kuhisi zaidi kiasi, mfano wa mtu ambaye ana shambulio la neva, kama mtu asiyejiweza ambaye amekaa kitandani kwa miaka mingi. Kuwafanya kuwa wagumu katika imani yao kwa maneno ya Mungu, mara nyingi Mungu anasisitiza yafuatayo: “Ili kwamba hatua inayofuata ya kazi Yangu iweze kuendelea taratibu na bila kizuizi, Ninatumia usafishaji wa maneno kuwajaribu wale wote ambao wapo katika nyumba Yangu.” Hapa, Mungu anasema “kuwajaribu wale wote ambao wapo katika nyumba Yangu”; usomaji wa makini wa maneno haya hutuambia kwamba watu wanapofanya kazi kama watoa huduma, bado ni watu ndani ya nyumba ya Mungu. Aidha, maneno haya husisitiza hali ya ukweli ya Mungu kwa cheo cha “watu wa Mungu,” yakiwaleta watu kipimo cha unafuu katika mioyo yao. Na hivyo kwa nini Mungu huonyesha kwa kurudiarudia ufunuo mwingi kwa watu baada ya wao kusoma maneno ya Mungu, au wakati ambapo neno “watu wa Mungu” halijafichuliwa bado? Ni kuonyesha tu kwamba Mungu ni Mungu ambaye anaangalia ndani kabisa ya moyo wa mwanadamu? Hii ni sehemu tu ya sababu—na hapa, ni umuhimu tu wa pili. Mungu hufanya hivyo ili kuwafanya watu wote kushawishika kabisa, ili kwamba kila mtu, kutoka kwa maneno ya Mungu, aweze kuelewa udhaifu wake mwenyewe, na kujua mapungufu yake ya wakati uliopita kuhusiana na maisha, na, muhimu zaidi, ili kuweka msingi kwa ajili ya hatua ya kazi inayofuata. Watu wanaweza kujitahidi tu kumjua Mungu na kutaka kumuiga Mungu tu kwa msingi wa kujijua wenyewe. Kwa sababu ya maneno haya, watu hubadilika kutoka kuwa watu hasi na wa kutoonyesha hisia na kuwa na mtazamo mwema na wa kufanya vitendo, na hii huweka mizizi ya sehemu ya pili ya kazi ya Mungu. Inaweza kusemwa kwamba, kwa hatua hii ya kazi kama msingi, sehemu ya pili ya kazi ya Mungu inakuwa rahisi, ikihitaji jitihada kidogo tu. Hivyo, wakati watu huondoa huzuni mioyoni mwao na kuwa wenye mtazamo mwema na wa kufanya vitendo, Mungu huitumia vizuri fursa hii ili kufanya matakwa mengine kwa watu Wake: “Maneno Yangu yanatolewa na kuonyeshwa wakati wowote au mahali popote, na hivyo, nyinyi pia, mnapaswa kujijua wenyewe mbele Yangu wakati wote. Kwani leo ni, hata hivyo, tofauti na kile kilichokuja kabla, na hamwezi tena kutimiza chochote mnachotamani. Badala yake, kwa

kuongozwa na maneno Yangu, mnapaswa kuweza kuidhibiti miili yenu, mnapaswa kutumia maneno Yangu kama nguzo, na hampaswi kutenda kizembe.” Katika hili, Mungu kimsingi husisitiza “maneno Yangu”; wakati uliopita, pia, Alirejelea “maneno Yangu” mara nyingi, na hivyo, kila mtu hana budi ila kuelekeza uangalifu wake fulani katika hili. Ndivyo kiini cha hatua inayofuata ya kazi ya Mungu kinaonyeshwa: Watu wote watalazimika kuelekeza uangalifu wao kwa maneno ya Mungu, na wasiwe na upendo wowote mwingine. Wote wanapaswa kuyathamini maneno yote yanayotoka kwenye kinywa cha Mungu, na si kuyachezea, na hivyo hali iliopita itakuwa imekomeshwa kanisani, wakati mtu angesoma maneno ya Mungu na wengi wangesema amina na kuwa watiifu. Wakati huo, watu hawakujua maneno ya Mungu, lakini waliyachukua kama silaha ya kujilinda wenyewe. Kubadilisha hili, Mungu duniani hufanya matakwa mapya na ya juu kwa mwanadamu. Kuwazuia watu wasiwe hasi na watu wasio wa kuonyesha hisia baada ya kuona viwango vya juu vya Mungu na matakwa magumu, Mungu huwatia moyo watu mara nyingi kwa kusema: “Kwa kuwa mambo yamefikia hali ilivyo leo, hamhitaji kujihisi kutiwa uchungu na kujuta kuhusu matendo yenu ya zamani. Ukarimu Wangu hauna mipaka kama ilivyo bahari na anga—uwezo na ufahamu wa mwanadamu kunihusu Mimi unawezaje kukosa kujulikana Kwangu kama kiganja Changu?” Maneno haya ya kweli na ya dhati ghafula yanafungua akili za watu, na mara moja yanawaondoa katika hali ya kukata tamaa hadi kuwa na upendo kwa Mungu, kuwa wenye mtazamo mwema na wa kufanya vitendo, maana Mungu huzungumza kwa kukamata udhaifu ndani ya mioyo ya watu. Bila kutambua, watu siku zote wanaona haya mbele ya Mungu kwa sababu ya matendo yao ya zamani, na wao huonyesha majuto tena na tena. Hivyo, Mungu hufichua maneno haya hususan kwa uhalisia na kwa kawaida, ili kwamba watu wasihisi kwamba maneno ya Mungu ni magumu na hayana maisha, bali ni makali na laini, na ni dhahiri na kama yenye maisha.

Kuanzia uumbaji hadi leo, Mungu Amapanga kila kitu kwa ajili ya mwanadamu kimyakimya kuanzia ulimwengu wa kiroho, na kamwe hajaelezea ukweli wa ulimwengu wa kiroho kwa mwanadamu. Lakini, leo, ghafula Mungu anaelezea kwa muhtasari vita ambavyo vinaendelea vikali ndani yake, ambavyo kwa asili huwaacha watu wakikuna vichwa vyao, hukuza ufahamu wao kwamba Mungu ni wa maana sana na hawezi kueleweka, na hufanya iwe vigumu zaidi kwao kutambua chanzo cha maneno ya Mungu. Inaweza kusemwa kwamba hali ya kujihami ya ulimwengu wa kiroho huwaleta watu wote katika roho. Hii ni sehemu ya kwanza muhimu ya kazi ya baadaye, na ni dokezo tu ambalo kwalo watu wanaweza kuingia katika ulimwengu wa kiroho. Kutoka kwa hili inaweza kuonekana kwamba hatua inayofuata ya kazi ya Mungu imelengwa hasa roho, lengo la msingi ambalo ni kuwapa watu wote ufahamu mkubwa zaidi wa matendo ya kimiujiza ya Roho wa Mungu ndani ya mwili, hivyo kuwapa wale wote ambao ni watiifu kwa Mungu ufahamu mkubwa wa ujinga wa Shetani na asili ya Shetani.

Ingawa hawakuzaliwa katika ulimwengu wa kiroho, wanahisi kana kwamba wamemtazama Shetani, na mara wanapokuwa na hisia hii, Mungu mara moja Anabadilisha kwenda kwa njia nyingine ya kuzungumza—na mara watu wanapokuwa wamepata njia hii ya kufikiri, Mungu huuliza: “Kwa nini Ninawafundisha kwa hali hiyo ya dharura? Kwa nini Ninawaelezea ukweli wa ulimwengu wa kiroho? Kwa nini Ninawakumbusha na kuwaonya mara kwa mara?” Na kadhalika—mfululizo kamili wa maswali yanayoamsha maswali mengi katika akili za watu: Kwa nini Mungu huzungumza katika toni hii? Kwa nini Huzungumza masuala ya ulimwengu wa kiroho, na si matakwa Yake kwa watu katika kipindi cha kujenga kanisa? Kwa nini Mungu hagongi kwenye dhana za watu kwa kufichua siri? Kwa kutafakari kidogo zaidi tu, watu wanapata ufahamu mdogo wa hatua za kazi ya Mungu, na hivyo, wanapokumbana na majaribu hapo baadaye, ndani yao kunazaliwa maana halisi ya kumchukia Shetani. Na hata wanapokabiliana na majaribu hapo baadaye, bado wanaweza kumjua Mungu na kumchukia Shetani kwa kina zaidi, na hivyo kumlaani Shetani.

Mwishoni, mapenzi ya Mungu yote yanafichuliwa kwa mwanadamu: “kuruhusu kila maneno Yangu kukita mzizi kustawi na kuzaa matunda ndani ya roho zenu, na muhimu zaidi kuzaa matunda zaidi. Hiyo ni kwa sababu kile ninachokiomba si maua angavu yaliyostawi sana, bali matunda mengi—matunda, zaidi ya hayo, ambayo hayaharibiki.” Kati ya matakwa ya mara kwa mara ya Mungu kwa watu Wake hili ndilo pana zaidi kwa yote, ni hoja kuu, na limepelekwa mbele kwa njia iliyo ya moja kwa moja. Nimebadilika kutoka kufanya kazi katika ubinadamu wa kawaida hadi kufanya kazi katika uungu kamili; hivyo, katika wakati uliopita, katika maneno Yangu yaliyosemwa waziwazi, hakukuwa na haja Kwangu kuongeza ufafanuzi zaidi, na watu wengi sana waliweza kuelewa maana ya maneno Yangu. Matokeo yalikuwa ni kwamba, hapo nyuma, yale yote ambayo yalikuwa yanahitajika ni watu kuyajua maneno Yangu na waweze kuzungumza juu ya uhalisia. Hata hivyo, hatua hii, ni tofauti kwa kiasi kikubwa. Uungu Wangu unafanya kazi kabisa, na haujaacha nafasi kwa ubinadamu kuwa mshirika. Hivyo, ikiwa wale miongoni mwa watu Wangu wanatamani kuelewa maana ya kweli ya maneno Yangu, wana shida kubwa sana. Ni kupitia tu matamshi Yangu, ndipo wanaweza kupata mwanga na nuru, na ikiwa si kupitia njia hii, mawazo yoyote ya kuelewa malengo ya maneno Yangu ni ndoto tu bure za mchana. Watu wote watakapokuwa na ufahamu mkubwa zaidi kuhusu Mimi baada ya kukubali matamshi Yangu ni wakati ambapo watu Wangu kuishi kulingana na Mimi, ni wakati ambapo kazi Yangu katika mwili imekamilika, na wakati ambapo uungu Wangu unaishi kwa kudhihirishwa kabisa katika mwili. Wakati huu, watu wote watanitambua Mimi katika mwili, na kweli wataweza kusema kwamba Mungu huonekana katika mwili, na hili litakuwa ndilo tunda. Huu ni ushahidi zaidi kwamba Mungu amechoshwa na ujenzi wa kanisa—yaani, “Ingawa maua katika nyumba ya kioo ya kuhifadhi mimea ni yasiyohesabika kama nyota, na huwavuta watalii

wote, mara yanaponyauka yanakuwa mabovu mabovu kama hila danganyifu za Shetani, na hakuna mtu anayevutiwa nayo.” Ingawa Mungu Mwenyewe pia Alifanya kazi wakati wa kipindi cha ujenzi wa kanisa, kwa kuwa Yeye ni Mungu ambaye siku zote ni mpya, na kamwe si mzee, Hana hamu ya mambo yaliyopita. Kuwazuia watu kukumbuka nyakati za nyuma, Alitumia maneno “yanakuwa mabovu mabovu kama hila danganyifu za Shetani,” kitu kinachoonyesha kwamba Mungu hatii mafundisho ya dini. Baadhi ya watu wanaweza kufasiri vibaya mapenzi ya Mungu, na kuuliza: Kama ni kazi iliyofanywa na Mungu, kwa nini Alisema “mara yanaponyauka, hakuna mtu anayevutiwa nayo”? Maneno haya huwapatia watu ufunuo. Jambo la muhimu zaidi ni kwamba huwafanya watu wote kuwa na mwanzo mpya na sahihi, na baada ya hapo tu ndipo wataweza kuyaridhisha mapenzi ya Mungu. Hatimaye, watu wa Mungu wataweza kumpatia Mungu sifa ambayo ni ya kweli, si ya kulazimishwa, na ambayo inatoka mioyoni mwao. Hiki ndicho kipo katika kiini cha mpango wa Mungu wa usimamizi wa miaka 6,000. Yaani, ni udhihirisho wa mpango huu wa usimamizi wa miaka 6,000: kuwafanya watu wote kujua umuhimu wa kupata mwili kwa Mungu—kuwafanya kumjua Mungu kupata mwili kwa vitendo, ambayo ni kusema, matendo ya Mungu katika mwili—ili kwamba wamkane Mungu asiye yakini, na kumjua Mungu ambaye ni wa leo na pia wa jana, na zaidi ya hilo, Mungu wa kesho, ambaye kwa kweli Ameishi toka milele hadi milele. Ni baada ya hapo tu, ndipo Mungu ataingia pumzikoni!

Sura ya 4

Ili kuwazuia watu wote kutiwa kiburi na kujisahau baada ya mabadiliko yao kutoka kwa ubaya hadi kwa uzuri, katika sura ya maneno la mwisho la matamshi ya Mungu, mara tu Mungu akishazungumza kuhusu matakwa yake ya juu zaidi kwa watu Wake—mara tu Mungu akishawaambia watu kuhusu mapenzi Yake katika hatua hii ya mpango wa usimamizi Wake—Mungu huwapa nafasi ya kuyatafakari maneno Yake, kuwasaidia kufanya uamuzi wa kuridhisha mapenzi ya Mungu mwishowe. Wakati ambapo hali za watu ni nzuri, Mungu huanza mara moja kuwauliza watu maswali kuhusu upande mwingine wa suala. Yeye huuliza mfululizo wa maswali ambayo ni magumu kwa watu kuyaelewa: “Je, upendo wenu Kwangu ulikuwa umetiwa doa na uchafu? Je, uaminifu wenu Kwangu ulikuwa safi na wa moyo wako wote? Je, ufahamu wenu kunihusu ulikuwa wa kweli? Je, Nilikuwa na nafasi kiasi gani katika nyoyo zenu?” Na kadhalika. Katika nusu ya kwanza ya aya hii, isipokuwa kemeo mbili, yaliyobaki yote ni maswali. Hasa, “Je, matamshi Yangu yamewagonga katika sehemu yenu ya udhaifu?” ni swali la kufaa sana, na lile linalogonga kweli mambo ya siri kabisa ndani ya vina vya mioyo ya watu, kuwafanya kujiuliza wenyewe bila kufahamu: Je, mimi ni mwaminifu kweli katika upendo wangu kwa Mungu? Ndani ya mioyo yao, watu hukumbuka bila kufahamu uzoefu wao wa wakati uliopita katika kuhudumu: Waliharibiwa na kujisamehe, kujidai, kujiona, majisifu, ridhaa

kupita kiasi, na kiburi. Walikuwa kama samaki mkubwa aliyenaswa ndani ya wavu—na baada ya kuingia ndani ya nyavu hizi, haikuwa rahisi kwao kujinasua. Na zaidi ya hayo, walikuwa wasiozuiwa mara kwa mara, walidanganya mara kwa mara ubinadamu wa kawaida wa Mungu, na wakajithamini wenyewe katika yote waliyofanya. Kabla ya kuitwa “watendaji huduma,” walikuwa kama mtoto wa chui mkubwa mwenye milia aliyezaliwa, aliyejawa nguvu. Ingawa kwa kiasi walilenga uangalifu wao kwa uzima, wakati mwingine walifanya mambo kwa namna isiyo ya dhiti; kama mtumwa, walikuwa wazembe kwa Mungu. Katika wakati wa kufichuliwa kama watendaji huduma, walikuwa wabaya, walibaki nyuma, walijawa na huzuni, walilalamika kuhusu Mungu, waliinamisha vichwa vyao kwa huzuni, na kadhalika. Kila hatua ya hadithi zao wenyewe za ajabu, na za kugusa moyo hukawia ndani ya fikira zao. Hata inakuwa vigumu kwao kulala, na wao hushinda mchana katika mzubao. Wanaonekana kwamba wameondolewa mara ya pili na Mungu, wameanguka Kuzimu, na hawana uwezo wa kutoroka. Ingawa Mungu hakufanya chochote ila kuuliza maswali machache magumu katika aya ya kwanza, soma kwa makini, yanaonyesha kwamba lengo la Mungu ni zaidi ya kuuliza tu haya maswali kwa ajili ya wao wenyewe; ndani yao kuna kiwango cha kina cha maana, kile ambacho ni lazima kielezwe kwa utondoti mkuu zaidi.

Ni kwa nini Mungu alisema wakati fulani kwamba leo, hata hivyo, ni leo, na kwa vile jana tayari imepita, hakuna wito wa kiu ya mambo yaliyozeewa, na ilihali katika sentensi ya kwanza hapa, Anawauliza watu maswali, na kuwasababisha wakumbuke wakati uliopita? Hebu fikiria: Ni kwa nini Mungu anasema kwamba watu wasiwe na kiu ya mambo yaliyozeewa kuhusu wakati uliopita, lakini pia wayakumbuke? Inawezekana kwamba kuna makosa katika maneno ya Mungu? Inawezekana kwamba asili ya maneno haya ina makosa? Kwa kawaida, wale wasiozingatia maneno ya Mungu hawangeweza kuuliza maswali ya kina kama hayo. Lakini kwa wakati huu, hakuna haja ya kulizungumzia hili. Kwanza, wacha Nieleze “kwa nini” ya hapo juu. Bila shaka, kila mtu anafahamu kwamba Mungu amesema Yeye haneni maneno matupu. Maneno yakitamkwa kutoka kinywani mwa Mungu, basi kuna lengo na umuhimu kwayo—na hili linagusa kiini cha suala. Kasoro kubwa zaidi ya watu ni kutoweza kwao kubadilisha njia zao za uovu na utatanishi wa asili yao ya zamani. Kuwakubalia watu wote kujijua kabisa na kwa uhalisi, Mungu kwanza anawaongoza kukumbuka wakati uliopita, ili waweze kufikiri juu yao wenyewe kwa kina, na hivyo waje kujua kwamba hakuna hata neno moja la Mungu lililo tupu, na kwamba maneno yote ya Mungu hutimizwa katika watu tofautitofauti kwa viwango tofautitofauti. Katika wakati uliopita, namna ambayo Mungu aliwashughulikia watu iliwapa ufahamu kidogo wa Mungu na kusababisha uaminifu wao kwa Mungu kuwa wa dhiti zaidi kidogo. Neno “Mungu” linachukua asili mia 0.1 pekee ndani ya watu na mioyo yao. Kutimiza hili kunaonyesha Mungu ametekeleza kiasi kikubwa mno cha wokovu. Ni haki kusema kwamba

kutimiza kwa Mungu kwa kiasi hiki katika kundi hili la watu—kundi linalonyonywa na joka kuu jekundu na kutawaliwa na Shetani—ili wasithubutu kufanya wapendavyo. Hiyo ni kwa sababu haiwezekani kwa Mungu kumiliki asilimia mia moja ya mioyo ya wale ambao wametawaliwa na Shetani. Ili kuongeza ufahamu wa watu kuhusu Mungu wakati wa hatua inayofuata, Mungu analinganisha hali za watendaji huduma wa zamani na zile za watu wa Mungu wa leo, hivyo kuunda tofauti wazi inayoongeza hisi ya watu ya aibu. Kama alivyosema tu Mungu, “hamna mahali pa kuficha aibu yenu?”

Kwa hiyo, mbona Nilisema kwamba Mungu haulizi tu maswali kwa ajili ya hayo yenyewe? Kusoma kwa makini kuanzia mwanzo hadi mwisho kunaonyesha kwamba, ingawa maswali yanayoulizwa na Mungu hayajaelezwa kabisa, yote yanahusu kiasi cha uaminifu wa watu kwa Mungu na ufahamu wa Mungu; yanahusu, kwa maneno mengine, hali halisi za watu, ambazo ni za kusikitisha, na ngumu kwao kueleza wazi kuzihusu. Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba kimo cha watu ni cha kimbaombao sana, kwamba ufahamu wao wa Mungu ni wa juujuu sana, na uaminifu wao Kwake ni wa mawaa na najisi sana. Kama alivyosema Mungu, karibu watu wote hufanya mambo magumu ili kujinufaisha na wako pale tu kuongeza idadi. Mungu anaposema “Je, mnaamini kwa kweli kuwa hamjafuzu kuwa watu Wangu?” maana ya kweli ya maneno haya ni kwamba miongoni mwa watu wote, hakuna wanaofaa kuwa watu wa Mungu. Lakini ili kutimiza athari kubwa zaidi, Mungu hutumia mbinu ya kuuliza maswali. Mbinu hii ni ya kufaa zaidi kuliko maneno ya wakati uliopita, ambayo kwa kikatili yalishambulia, yakakatakata, na kuwaua watu, kiasi cha kuumiza mioyo yao. Tuseme Mungu angekuwa amesema moja kwa moja jambo la kuchosha na lisilo na ladha kama “Ninyi si waaminifu Kwangu, na uaminifu wenu ni wa mawaa, na Sishikilii mahali halisi ndani ya mioyo yenu.... Sitakuachia mahali pa wewe kujificha kutoka kwako mwenyewe, kwani hakuna kati yenu anayetoshwa kuwa watu Wangu.” Mnaweza kulinganisha mawili: Maudhui yake ni sawa, lakini toni ya kila moja ni tofauti. Kutumia maswali ni kwa kufaa zaidi. Hivyo, Mungu mwenye hekima anatumia toni ya kwanza, ambayo inaonyesha ustadi Anaotumia kuzungumza. Hili haliwezi kutimizwa na mwanadamu, na hivyo sio ajabu kwamba Mungu alisema, “Watu ni vyombo tu wanaotumiwa na Mimi, tofauti pekee iliyoko kati yao ni kwamba wengine ni duni, na wengine ni wa thamani.”

Endeleeni kusoma. Maneno ya Mungu huja kwa idadi kubwa na haraka, na kuwapa watu nafasi ya kupumua kwa shida, kwani Mungu hawi mwangalifu kwa mwanadamu kamwe. Watu wanapohisi majuto makubwa sana, Mungu huwaonya kwa mara nyingine: “Iwapo hutambui kabisa maswali haya, basi hii inaashiria kuwa unafanya kazi gizani, kwamba uko tu pale kuongeza idadi, na kwamba katika muda ulioamuliwa na Mimi kabla ya siku hii, kwa hakika utaangamizwa na kutupwa katika shimo lisilo na mwisho kwa mara ya pili. Haya ni maneno

Yangu ya onyo, na yeyote anayeyachukulia kwa wepesi atapigwa na hukumu Yangu, na, kwa wakati ulioteuliwa atapatwa na janga.” Kuyasoma maneno hayo, watu hawawezi kufanya lolote ila kufikiria juu ya wakati ambapo walitupwa ndani ya shimo lisilo na mwisho: Kwa kutishwa na msiba mkuu, kutawaliwa na amri za usimamizi za Mungu, mwisho wao wenyewe ukiwangoja, kwa muda mrefu wakihihi kusikitishwa, wenye huzuni, wasiotulia, wasioweza kumwambia yeyote kuhusu ghamu iliyo ndani ya mioyo yao—yakilinganishwa na hili, ingekuwa heri kwao ikiwa wangeacha miili yao itakaswe.... Wakilifikiria hili, hawana la kufanya ila kuhisi kusikitishwa. Wakifikiria kuhusu vile walikuwa wakati uliopita, vile walivyo leo, na vile watakavyokuwa kesho, huzuni ndani ya mioyo yao hukua, wao huanza kutetemeka bila kufahamu, na hivyo wao huogopa zaidi amri za usimamizi za Mungu. Inavyotokea kwao kwamba neno “Watu wa Mungu” linaweza pia kuwa njia ya kuzungumza, furaha ndani ya mioyo yao hugeuka mara moja kuwa sikitiko. Mungu anatumia udhaifu wao wa mauti kuwapiga, na wakati huu, Anaanza hatua inayofuata ya kazi Yake, akisababisha hisia za uchangamfu kuzidi kuamshwa, na kuongeza hisi yao kwamba matendo ya Mungu ni yasioeleweka, kwamba Mungu hafikiki, kwamba Mungu ni mtakatifu na safi, na kwamba hawastahili kuwa sehemu ya watu wa Mungu. Kutokana na hilo, wanaongeza maradufu juhudi zao za kujiendeleza wenyewe, hawathubutu kubaki nyuma.

Linalofuata, ili kuwafunza watu funzo, na kuwafanya wajijue wenyewe, kumcha Mungu, na kumwogopa Mungu, Mungu huanza mpango Wake mpya: “Tangu wakati wa uumbaji mpaka sasa, watu wengi wamekosa kutii maneno Yangu na hivyo wametupwa nje na kutolewa katika mtiririko wa urejesho Wangu; hatimaye, miili yao inaangamia na roho zao zinatupwa kuzimu, na mpaka wa leo bado wanapitia adhabu kali. Watu wengi wameyafuata maneno Yangu, lakini wameenda kinyume na nuru na mwanga Wangu ... na wengine....” Hii ni mifano halisi. Katika maneno haya, Mungu hawapi tu watu wote wa Mungu onyo halisi la kuwafanya wayajue matendo ya Mungu kotekote katika enzi, bali pia hutoa ufafanuzi usio wazi wa sehemu ya kile kinachofanyika katika ulimwengu wa kiroho. Hili linawakubalia watu kujua kwamba hakuna kizuri kinachoweza kutokana na wao kutomtii Mungu. Watakuwa alama ya milele ya aibu, na watakuwa mfano halisi wa Shetani, na nakala ya Shetani. Ndani ya moyo wa Mungu, hali hii ya maana ni ya umuhimu wa baadaye, kwani maneno haya tayari yamewaacha watu wakitetemeka na wakiwa na hasara. Uzuri wa hili ni kwamba, watu wanapotetemeka kwa woga, wao pia hupata kiasi fulani cha tondoti za ulimwengu wa kiroho—lakini kiasi fulani tu, kwa hiyo lazima Nitoe ufafanuzi kidogo. Kutoka kwa mlango wa ulimwengu wa kiroho inaweza kuonekana kwamba kuna aina zote za pepo. Wengine, hata hivyo, wako Kuzimu, wengine wako jehanamu, wengine wako katika ziwa la moto, na wengine wako ndani ya shimo lisilo na mwisho. Nina kitu fulani cha kuongeza hapa. Kuzungumza kwa kijuujuu, pepo hawa wanaweza kugawanywa

kulingana na mahali; kuzungumza kwa dhahiri, hata hivyo, wengine wanashughulikiwa moja kwa moja na kuadibu kwa Mungu, na wengine wako katika kifungo cha Shetani, anayetumiwa na Mungu. Kwa dhahiri zaidi, a kwao kunatofautiana kulingana na uzito wa hali zao. Wakati huu, wacha Nieleze zaidi kidogo. Wale wanaoadhibiwa moja kwa moja kwa mkono wa Mungu hawana roho duniani, kumaanisha hawana nafasi ya kuzaliwa upya. Roho wanaomilikiwa na Shetani—maadui ambao Mungu huzungumzia Anaposema “kuwa adui Zangu”—wameunganishwa kwa mambo ya kidunia. Pepo wabaya mbalimbali walio duniani wote ni maadui wa Mungu, watumishi wa Shetani, na sababu yao ya kuwepo kwao kutoa huduma ili kuwa yenye upinzani kwa matendo ya Mungu. Hivyo, Mungu husema, “Watu hawa hawajafanywa tu wafungwa na Shetani, bali wamekuwa watenda dhambi wa milele na kuwa adui Zangu, na wananipinga moja kwa moja.” Linalofuata, Mungu huwaambia watu kuhusu mwisho wa aina hii ya pepo: “Watu wa aina hii ndio viumbe Nitakaohukumu wakati wa ghadhabu Yangu kali,” Mungu pia hubainisha hali zao za wakati huu: “leo hii wao bado ni vipofu, wakiwa bado ndani ya jela zenye giza.”

Ili kuwaonyesha watu ukweli wa maneno ya Mungu, Mungu hutumia mfano halisi kama thibitisho (suala la Paulo ambalo Anazungumzia) ili onyo Lake liweze kuacha kwa watu alama ya kina zaidi. Ili kuwakomesha watu kuchukulia kama hadithi kile kinachosemwa kuhusu Paulo, na kuwazuia kujifikiria kama watazamaji—na, zaidi ya hayo, ili kuwakomesha kwenda huku na huko wakijivunia mambo yaliyofanyika maelfu ya miaka iliyopita waliyojifunza kutoka kwa Mungu, Mungu hamakinikii matukio aliyopitia Paulo katika maisha yake yote. Badala yake, Mungu analenga juu ya matokeo na mwisho wa Paulo, sababu ambayo Paulo alimpinga Mungu, na vile Paulo aliishia kama alivyoishia. Kile ambacho Mungu analenga ni kusesitiza kanusho Lake la matumaini ya utukufu ya Paulo hapo mwisho, na kuweka wazi moja kwa moja hali yake katika uwanja wa kiroho: “Paulo anaadhibiwa moja kwa moja na Mungu.” Kwa sababu watu ni wasiosikia na hawana uwezo wa kuelewa chochote cha maneno ya Mungu, Mungu anaongeza ufafanuzi (sehemu inayofuata ya matamshi), na kuanza kuzungumza kuhusu suala la eneo lingine: “yeyote anayeniasi (na sio kuuasi tu mwili Wangu lakini la muhimu zaidi, maneno Yangu na Roho Wangu, ambayo ni kusema uungu Wangu), anapata hukumu Yangu katika mwili wake.” Ingawa, kwa kuzungumza kijuujuu, maneno haya yanaonekana kutokuwa na uhusiano na yale yaliyo hapo juu, na inaonekana hakuna uhusiano wowote kati ya hayo mawili, msiwe na hofu: Mungu ana malengo Yake mwenyewe; maneno rahisi ya “mfano ulio hapo juu yanathibitisha kwamba” yanaunganisha kimfumo masuala mawili yanayoonekana kutohusiana—ambayo ni ustadi wa maneno ya Mungu. Hivyo, watu wanapata nuru kupitia kwa maelezo ya Paulo, na kwa hiyo, kwa sababu ya uhusiano ulioko kati ya maneno halisi yaliyo hapo juu na hapa chini, ufuatiliaji wao wa kumjua Mungu huongezwa kupitia kwa somo la Paulo, ambalo

hasa ni athari ambayo Mungu alitaka kutimiza katika kuyazungumza maneno hayo. Linalofuata, Mungu anazungumza maneno mengine yanayotoa usaidizi na kupata nuru kwa kuingia kwa watu katika maisha. Haina haja ya Mimi kuingia katika hilo. Mtahisi kwamba ni rahisi kuyaelewa. Kila ambacho lazima Nieleze, hata hivyo, ni wakati ambapo Mungu anasema, “Nilipofanya kazi katika ubinadamu wa kawaida, watu wengi walikuwa tayari wamejipima dhidi ya ghadhabu Yangu na uadhama Wangu, na tayari walijua kiasi kidogo kuhusu hekima na tabia Yangu. Leo hii, Ninazungumza na kutenda moja kwa moja katika uungu, na bado kuna baadhi ya watu ambao wanaona ghadhabu na hukumu Yangu kwa macho yao wenyewe; zaidi ya hayo, kazi muhimu ya sehemu ya pili ya enzi ya hukumu ni kuwafanya watu Wangu wote wajue matendo Yangu katika mwili moja kwa moja, na kuwafanya ninyi nyote mtazame tabia Yangu moja kwa moja.” Maneno haya machache yanahitimisha kazi ya Mungu katika ubinadamu wa kawaida na kuanzisha rasmi sehemu ya pili ya kazi ya Mungu ya enzi ya hukumu, inayotekelezwa katika uungu, na kutabiri mwisho wa sehemu ya watu. Wakati huu, inastahili kueleza kwamba Mungu hakuwaambia watu kwamba hii ilikuwa sehemu ya pili ya enzi ya hukumu walipokuwa watu wa Mungu. Badala yake, baada tu ya kuwaambia watu kuhusu mapenzi ya Mungu na malengo ambayo Mungu hutamani kutimiza wakati wa kipindi hiki, na kuhusu hatua ya mwisho ya Mungu ya kazi duniani ndipo Anaeleza kwamba hii ni sehemu ya pili ya enzi ya hukumu. Ni wazi kwamba, pia kuna hekima ya Mungu katika hili. Watu wakishaamka tu kutoka kwa vitanda vyao vya wagonjwa, kitu cha pekee ambacho wanajali ni kama watakufa au la, au kama ugonjwa wao unaweza kuondolewa ndani yao au la. Hawatili maanani kama wataongeza uzito, au kama wanavalia nguo sawa. Hivyo, ni wakati tu ambapo watu wanaamini kabisa kwamba wao ni sehemu ya watu wa Mungu ndipo Mungu huzungumza juu ya matakwa Yake, hatua kwa hatua, na Huwaambia watu enzi ya leo ni gani. Hiyo ni kwa sababu watu huwa tu na nguvu za kutilia maanani hatua za usimamizi wa Mungu siku chache baada ya wao kupata nafuu, na kwa hiyo huu ni wakati wa kufaa zaidi wa kuwaambia. Ni baada tu ya watu kuelewa ndipo wanaanza kuchambua: Kwa vile hii ni sehemu ya pili ya enzi ya hukumu, matakwa ya Mungu yamekuwa makali zaidi, na Nimekuwa mmoja wa watu wa Mungu. Ni sawa kuchambua hivyo, linafikika na mwanadamu, na hivyo Mungu hutumia mbinu hii ya kuzungumza.

Mara tu watu wanapoelewa kidogo, Mungu mara tena huingia katika ufalme wa kiroho kuzungumza, na hivyo wao mara tena huingia katika uvamizi. Wakati wa mfululizo huu wa maswali, kila mtu hujikuna kichwa chake, akichanganyikiwa, asijue mapenzi ya Mungu yako wapi, asijue ni maswali gani ya Mungu atayajibu, na, aidha, asijue ni lugha gani ya kutumia kuyajibu maswali ya Mungu. Mtu hushangaa kama atacheka au atalia. Kwa watu, maneno haya yanaonekana kama kwamba yanaweza kuwa na mafumbo makubwa sana—lakini ukweli ni kinyume kabisa. Huenda hata Nikakuongezea ufafanuzi kidogo hapa- hii itaipa akili yako

pumziko, na utahisi ya kuwa hiki ni kitu rahisi na hakuna haja ya kulifikiria juu yake. Kwa kweli, ingawa kuna maneno mengi, yana lengo moja tu la Mungu: kuupata uaminifu wa watu kupitia maswali haya. Lakini si la kufaa kusema hili moja kwa moja, kwa hiyo Mungu anatumia maswali mara nyingine tena. Toni, hata hivyo, ni nyororo hasa, tofauti kabisa na hapo mwanzo. Ingawa wanaulizwa maswali na Mungu, aina hii ya utofautishaji huwaletea watu kiwango fulani cha tulizo. Waweza basi ukasoma kila swali moja kwa moja; je, mambo haya hayakuwa yakitajwa mara kwa mara wakati uliopita? Kaika maswali haya machache rahisi, kuna maudhui mengi. Mengine ni maelezo ya fikira za watu: “Je, uko radhi kuyafurahia maisha hapa duniani ambayo yanafanana na yale yaliyo mbinguni?” Mengine ni “kiapo cha askari wa vita” cha watu mbele ya Mungu: “Je, kweli mna uwezo wa kujiruhusu kuuwawa na Mimi, na kuongozwa na Mimi, kama kondoo?” Na mengine ni matakwa ya Mungu kwa mwanadamu: “Kama Singezungumza moja kwa moja, je, ungewacha kila kitu kilicho karibu na wewe na ukubali kutumiwa na Mimi? Je, hii siyo hali halisi Ninayohitaji ...?” Au ushawishi na uthibitisho za Mungu kwa mwanadamu: “Ilhali Ninauliza kuwa msishushwe na wasiwasi tena, kwamba muwe msitari wa mbele katika kuingia kwenu na muelewe kiini cha maneno Yangu. Hii itazuia hali ya nyinyi kutoelewa maneno Yangu, na hali ya kutokuwa na uwazi kuhusu maana Yangu, na hivyo kukiuka amri Zangu za utawala.” Hatimaye, Mungu anazungumza kuhusu matumaini yake kwa mwanadamu: “Natumaini kuwa mtaelewa Nia Yangu kwenu katika maneno Yangu. Msifikiri juu ya matarajio yenu tena, na mtende vile ambavyo mmeamua mbele Yangu kutii mipango ya Mungu katika kila kitu.” Swali la mwisho lina maana ya kina. Ni la kuchochea akili, linaathiri mioyo ya watu na ni gumu kulisahau, linalia bila kukoma kama kengele inayoning’inia karibu na masikio yao ...

Yaliyo hapo juu ni maneno machache ya ufafanuzi kwa wewe kutumia kama rejaleo.

Sura ya 5

Mungu anapoweka mahitaji kwa wanadamu ambayo ni magumu kwao kueleza, na maneno Yake yanapogonga moja kwa moja katika moyo wa mwanadamu na watu wanatoa mioyo yao ya dhati ili Afurahie, basi Mungu huwapa watu nafasi ya kutafakari, kufanya uamuzi, na kutafuta njia ya kutenda. Kwa njia hii, wote ambao ni watu Wake kwa mara nyingine, ngumi zikiwa zimekunjwa kwa ujasiri, watatoa nafsi zao zote kwa Mungu. Baadhi, labda, wanaweza kuunda mpango na kuanzisha ratiba ya kila siku, wanapojiandaa kujisisimua na kwenda kazini, wakitoa sehemu yao ya nguvu kwa mpango wa usimamizi wa Mungu, ili kuleta utukufu kwa mpango huu na kuharakisha hitimisho lake. Na, kama vile watu wanavyojipata katika hali hii ya kisaikolojia, wakashikilia mambo haya kwa karibu akilini mwao wakati wanapokuwa wakiendelea na kazi zao, wanapozungumza, na wanapokuwa wakifanya kazi, Mungu, kwa haraka akifuatilia hili,

Huanza kusema tena: “Wakati Roho Wangu anatoa sauti, anaonyesha hali nzima ya tabia Yangu. Je, nyinyi mnalifahamu hili?” Kadri mwanadamu alivyo na uamuzi zaidi, ndivyo atakavyokuwa na tamaa zaidi ya kufahamu mapenzi ya Mungu na ndivyo atakavyotamani kwa ari zaidi Mungu aweke madai kwake; na hivyo Mungu atawapa watu kile ambacho wanataka, Akitumia fursa hii kutoa maneno Yake, yaliyokuwa yamewekwa tayari kwa muda mrefu, kwa maficho ya ndani kabisa ya nafsi zao. Ingawa maneno haya yanaweza kuonekana kuwa makali au ya kukwaruza kiasi, kwa binadamu ni matamu zaidi kulinganishwa na kitu chochote. Mara moja, moyo unachanua kwa furaha, kana kwamba binadamu wako mbinguni, au wamepelekwa katika ulimwengu mwingine, paradiso ya hakika ya mawazo, ambako mambo ya nje ya ulimwengu hayawaathiri tena binadamu. Ili kwamba watu wasizungumze tena, kama walivyokuwa na tabia ya kufanya zamani, kwa nje na kutenda kwa nje, na hivyo kushindwa kuweka misingi wa kufaa: ili kuiepuka hatima hii, wakati kile ambacho watu wanatamani mioyoni mwao kimefanikiwa, na zaidi wanapojiandaa kwenda kazini kwa shauku kubwa, Mungu bado anabadili njia Yake ya kuzungumza kulingana na hali yao ya kisaikolojia, na, kwa ufupi na bila kujizuia, Hubainisha shauku yote na sherehe ya kidini ndani ya mioyo yao. Kama Mungu alivyosema: “Je, kweli mmeona umuhimu ulioko humu?” Ikiwa ni kabla au baada ya mwanadamu kuweka dhamira yake juu ya kitu fulani, haweki umuhimu mkubwa juu ya kumjua Mungu katika matendo Yake au kwa maneno Yake, lakini badala yake anaendelea kutafakari swali hili: “Ninaweza kumfanyia nini Mungu? Hilo ndilo suala muhimu!” Hii ndiyo maana Mungu anasema: “Na mna ujasiri wa kujiita watu Wangu usoni Mwangu—hamna hisia ya aibu, sembuse mantiki yoyote!” Mara tu baada ya Mungu kusema maneno haya, mara moja watu hutambua, na kana kwamba wamepatwa na mshtuko wa umeme, wanaharakisha kuificha mikono yao kwa vifua vyao, wakiwa na uoga mwingi kuchochea ghadhabu ya Mungu mara ya pili. Kuongezea kwa hili, Mungu amesema pia: “Siku moja, watu kama hawa watafukuzwa kutoka katika nyumba Yangu. Usithubutu kunidanganya, ukifikiri kwamba umesimama kwa ajili ya ushuhuda Wangu!” Wanaposikia maneno kama haya, watu wanaogopa hata zaidi, kama vile wangeogopa wakiwa wamemwona simba. Wanajua vizuri kabisa mioyoni mwao. Wao kwa upande mmoja wana wasiwasi wasiliwe na simba huku kwa upande mwingine wanahisi kutojua pa kutorokea. Wakati huu, mpango ndani ya moyo wa mwanadamu hupotea usionekane tena, kabisa na kikamilifu. Kupitia maneno ya Mungu, ninahisi kama kwamba ninaweza kuona kila kipengele cha aibu ya binadamu: Tabia ya kuinamisha kichwa na kuona aibu, kama mtahiniwa ambaye ameanguka mtihani wa kuingia chuo kikuu, maadili yake ya fahari sana, familia yenye furaha, siku za usoni zenye ufanisi, na kadhalika na kadhalika, yote yaligeuka—pamoja na Mipango Minne ya Kufanya kuwa ya Kisasa kabla ya Mwaka 2000—kuwa maongezi matupu, yakisababisha mandhari ya kufikirika katika filamu ya sayansi ya ubunifu. Hii ni ili kubadilishana mambo ya kukaa tu na yale ya utendaji kazi, kuwafanya watu, ndani ya kutojishughulisha kwao, kusimama mahali ambapo Mungu

amewaweka. Jambo muhimu la pekee ni ukweli kwamba wanadamu wanaogopa sana kupoteza cheo hiki; hivyo basi wanakwambia beji zao za ofisi kwa bidii yao yote, wakiwa na uoga mwingi kuwa mtu anaweza kujaribu kuzipokonya kutoka kwao. Wakati binadamu wako katika hali hii ya akili, Mungu hana wasiwasi kuwa watakuwa wenye kukaa tu, na kwa hiyo inavyostahili Yeye hubadili maneno Yake ya hukumu kuwa maneno ya kuhoji. Hawapi watu fursa ya kupunga hewa tu, lakini pia Anawapa fursa ya kuchukua matarajio waliyokuwa nao kabla ya sasa na kuyatayarisha kwa ajili ya kuyaangalia baadaye: Kile ambacho hakifai kinaweza kubadilishwa. Hii ni kwa sababu Mungu bado Hajaanza kazi Yake—hii ni bahati nzuri katikati ya bahati mbaya sana—na, zaidi ya hayo, Hawahukumu. Kwa hiyo acha niendeleo kumpa ibada yangu yote!

Halafu, hupaswi kamwe kwa sababu ya hofu yako, kuweka kando maneno ya Mungu. Angalia uone kama Mungu ana mahitaji yoyote mapya. Kwa hakika, utagundua aina hii ya mahitaji: “Kuanzia wakati huu na kuendelea, katika mambo yote lazima uingie katika ukweli wa kutenda; kupiga domo tu, kama ulivyokuwa ukifanya, hakutakusaidia tena.” Ndani yake pia kunadhihirishwa hekima ya Mungu. Mungu daima Amewalinda shahidi Wake mwenyewe, na wakati ukweli wa maneno ya zamani umefikia hitimisho lake, hakuna mtu yeyote anayeweza kufahamu ujuzi wa “ukweli wa kutenda.” Hii inatosha kuthibitisha ukweli wa kile ambacho Mungu alisema “Ninaanza kufanya kazi hiyo Mwenyewe.” Inahusiana na maana halisi ya kazi katika uungu, na pia inahusiana na sababu kwa nini wanadamu, baada ya kufikia hatua mpya ya mwanzo, bado hawawezi kuelewa maana halisi ya maneno ya Mungu. Hii ni kwa sababu, zamani, idadi kubwa ya watu wangeshikilia ukweli katika maneno ya Mungu, ilhali leo hawana ufahamu juu ya ukweli wa kutenda, lakini wanaelewa tu vipengele vya juu juu vya maneno haya bila kuelewa asili yao. Hata muhimu zaidi, ni kwa sababu leo, katika ujenzi wa ufalme, hakuna mtu anayeruhusiwa kuingilia kati, lakini kutii tu amri ya Mungu kama roboti. Kumbuka hili vizuri! Kila wakati ambao Mungu huleta mambo ya zamani, Yeye huanza kusema kuhusu hali halisi ya leo; hii ni namna ya kuzungumza ambayo inafanya tofauti kubwa sana kati ya kile kinachokuja kabla na kile kinachokuja baadaye, na kwa sababu hii inaweza kufikia matunda bora hata zaidi, ikiwawezesha watu kuiweka hali ya sasa sambamba na ile ya wakati uliopita, na kwa njia hii kuepuka kuchanganya tofauti iliyopo kati ya hizi mbili. Huu ni upande mmoja wa hekima ya Mungu, na lengo lake ni kufikia matunda ya kazi. Baada ya hili, Mungu kwa mara nyingine Hufichua ubaya wa wanadamu, ili kwamba binadamu hawatasahau kamwe kula na kunywa maneno ya Mungu kila siku, na hata muhimu zaidi ili kwamba kila siku watajijua na kuchukua hili kama somo ambalo wanapaswa kujifunza kila siku.

Anapomaliza kuzungumza maneno hayo, Mungu amefanikisha matokeo ambayo Alinulia awali. Na kwa hiyo, bila kujali zaidi kama binadamu wamemwelewa au la, Yeye huipitia hili upesi sana kwa maneno machache, kwa sababu kazi ya Shetani haina uhusiano wowote na

binadamu—kuhusu hili binadamu hawana ufahamu. Sasa, ukiacha ulimwengu wa roho, angalia zaidi jinsi Mungu anavyoweza mahitaji Yake kwa binadamu: “Ninapopumzika katika makaazi Yangu, Mimi huchunguza kwa karibu: Watu wote duniani wamo katika pilikapilika, ‘wakisafiri duniani kote’ na kukimbia huku na kule, yote kwa ajili ya hatima yao, maisha yao ya baadaye. Lakini hakuna hata mmoja ana nguvu ya kutosha kwa ajili ya kuujenga ufalme Wangu, hata nguvu kiasi ambayo mtu hutumia kuvuta pumzi.” Baada ya kubadilishana mambo haya ya kawaida na wanadamu, Mungu bado hajali kuwahusu, lakini Anaendelea kuzungumza kutoka kwa mtazamo wa Roho, na kwa njia ya maneno haya, Anafichua hali za jumla za maisha ya jamii ya wanadamu. Ni wazi kuona, kutokana na “kusafiri duniani kote” na “kukimbia huku na kule,” kwamba maisha ya binadamu hayana maudhui. Ingekuwa kwa ajili ya wokovu wenye nguvu wa Mungu, wale waliozaliwa katika familia ya chini na nje ya mstari wa kifalme wa China wangeishi maisha yote bure hata zaidi na ni heri waanguke Kuzimu na jahanamu kuliko kuja ulimwenguni. Chini ya utawala wa joka kuu jekundu, wao, bila kujua wenyewe, wamekosa dhidi ya Mungu na hivyo, kwa kawaida na tena bila kujua, wamekabiliwa na kuadibu kwa Mungu. Kwa sababu hii, Mungu amewachukua “waliookolewa kutokana na dhiki” na “wasio na shukrani” na kuwaweka pamoja kwa kuwalinganisha, kwamba wanadamu waweze kujitambua vizuri zaidi, na kuunda kutoka kwa hili foili kwa neema Yake ya kuokoa. Je! Hili halileti matokeo yanayofaa zaidi? Bila shaka, Sihitaji kusema kwa wazi sana, watu wanaweza, kutokana na yaliyomo katika mazungumzo ya Mungu, kuonyesha kipengele cha kukashifu, na tena, kipengele cha wokovu na rufaa, na hata tena, maonyesho mafupi ya huzuni. Wanaposoma maneno haya, watu bila kujua huanza kuhisi wenye mfadhaiko, na hawana budi ila kutoa machozi.... Lakini Mungu hatazuiliwa kwa sababu ya hisia chache za huzuni, wala Yeye, kwa sababu ya upotovu wa watu wote, Hataacha kazi Yake katika kuwafundisha watu Wake nidhamu na kuweka mahitaji kwao. Kwa sababu hii, mada Zake mara moja hugusia juu ya hali kama hizo za leo, na zaidi ya hayo Anatangaza kwa binadamu uadhama wa amri Zake za utawala, ili kwamba mpango Wake uendelee kwenda mbele. Hii ndiyo sababu, baada ya hili kwa kasi ya kutosha na kumkunja samaki angali mbichi, Mungu anatangaza wazi wakati huu muhimu katiba ya nyakati, katiba ambayo inapaswa kusomwa kwa uangalifu kwa karibu kwa kila kifungu kabla binadamu waweze kuelewa mapenzi ya Mungu. Hakuna haja ya kuingia zaidi katika hili sasa—lazima tu wasome kwa makini zaidi.

Leo, nyinyi—hili kundi la watu hapa—ndio pekee ambao mnaweza kuona kwa kweli maneno ya Mungu. Hata hivyo, katika kumjua Mungu, watu wa leo wamebaki nyuma sana ya mtu yeyote katika enzi zilizopita. Kutokana na hili ni wazi kabisa kiwango cha juhudi ambazo Shetani amewekeza kwa watu katika miaka hii elfu kadhaa, na kiwango ambacho zimewapotosha wanadamu, ambacho ni kikubwa sana kiasi kwamba, hata ingawa Mungu

amesema maneno mengi sana, bado binadamu hawamwelewi wala hawamjui Mungu, lakini badala yake wanathubutu kusimama na kumpinga hadharani. Na hivyo Mungu mara nyingi huwafanya watu wa zamani kuwa kama ulinganishi kwa watu wa leo, ili kuwapa watu wa leo, licha ya wao kuwa wasiohisi na wapumbavu, nafasi ya uhakika ya marejeo. Kwa sababu wanadamu hawana maarifa ya Mungu, na kwa sababu hawana imani ya kweli ndani Yake, Mungu amewahukumu binadamu kuwa hawana sifa na mantiki, na hivyo, mara kwa mara, Amewaonyesha watu uvumilivu na kuwapa wokovu. Pigano linapiganwa kwa njia hii katika ulimwengu wa roho: Ni tumaini lisilofanikiwa la Shetani kuwapotosha wanadamu kwa kiwango fulani, kuufanya ulimwengu kuwa mbaya na mwovu, na hivyo kumvuta mwanadamu ndani ya matope na kuuharibu mpango wa Mungu. Lakini mpango wa Mungu sio kuwafanya binadamu wote kuwa watu wanaomjua, bali badala yake kuchagua sehemu ya kuwakilisha yote, na kuacha wengine kama bidhaa taka, kama bidhaa zilizoharibika, wanaofaa kutupwa kwenye rundo la takataka. Na hivyo, ingawa kutoka kwa mtazamo wa Shetani kuwamiliki watu wachache kunaonekana kuwa fursa nzuri kabisa ya kuuharibu mpango wa Mungu, je, zuzu kama yeye anawezaje kujua kuhusu nia ya Mungu? Hii ndiyo maana Mungu alisema, zamani, “Nimeufunika uso Wangu ili kuepuka kuangalia ulimwengu huu.” Tunajua kidogo kuhusu hili, na Mungu hahitaji kuwa wanadamu wawe na uwezo wa kufanya chochote, badala yake kwamba watambue kile Anachofanya kama cha muujiza na kisichoweza kueleweka na kumcha sana katika mioyo yao. Ikiwa, kama mtu anavyofikiria, Mungu angemwadibu bila kujali hali, basi dunia nzima ingekuwa imeangamia kitambo. Je, si huku kungemaanisha kuanguka ndani ya mtego wa Shetani? Na hivyo Mungu hutumia maneno Yake tu kufikia matunda Aliyo nayo mawazoni; mara chache sana kuna ujio wa ukweli. Je! Huu sio mfano wa kile Alichosema: “Kama Singeonea huruma ukosefu wenu wa sifa za kustahili, mantiki, na ufahamu, basi nyote mngeangamia katika kuadibu Kwangu, kutokuwepo tena. Lakini hadi wakati kazi Yangu hapa duniani itakapomalizika, Nitabaki mwenye huruma kwa wanadamu?”

Sura ya 6

Binadamu wanapigwa bumbuazi kwa sababu ya matamshi ya Mungu wanapotambua kwamba Mungu amefanya kitendo kikubwa katika ulimwengu wa kiroho, kitu ambacho mwanadamu hawezi na ambacho Mungu Mwenyewe pekee ndiye Anaweza kufanikisha. Kwa sababu hii, Mungu mara tena anawasilisha maneno ya huruma kwa wanadamu. Mioyo ya watu inapojaa ukinzani, ikishangaa: “Mungu ni Mungu asiye na huruma au upendo, lakini badala yake Mungu aliyejitolea kuwaangusha binadamu; kwa hiyo mbona Atuonyeshe huruma? Yawezekana kwamba Mungu kwa mara nyingine amehamia kwa utaratibu?” wakati ambapo fikira hii, wazo hili huumbika ndani ya akili zao, wao hung’ang’ana kulishinda kwa nguvu zao zote. Hata hivyo, baada ya kazi ya Mungu kuendelea mbele kwa kiasi kingine cha wakati, Roho Mtakatifu

ameanza kazi kubwa katika kanisa, na kila mwanadamu ameanza kufanya kazi ili kutekeleza shughuli yake, kisha wakati huo binadamu wote wameingia katika utaratibu huu wa Mungu. Hili ni kwa sababu hakuna yeyote anayeweza kuona dosari yoyote ndani kile ambacho Mungu husema na kufanya, na kuhusu kile ambacho Mungu atafanya baada ya hapo kwa kweli, hakuna yeyote anayeweza kujua au hata kukikisia. Kama vile amesema Mungu kwa kinywa Chake Mwenyewe: “Kati ya watu wote wanaoishi chini ya mbingu, kuna yeyote ambaye hayuko ndani ya kiganja cha mkono Wangu? Kuna yeyote asiyetenda kufuatana na maagizo Yangu?” Lakini Nawapa ushauri kidogo: Katika masuala ambayo hamwelewi kabisa, yeyote kati yenu, asinene wala kutenda. Kile ambacho Nimesema sasa hivi sio ili kufyonza shauku yenu, bali kukuhimiza kufuata mwelekeo wa Mungu katika matendo yako. Kwa vyovyote vile, usife moyo au kuingia katika tashwishi, kwa sababu ya kile Nilichosema kuhusu “dosari”: Kusudi Langu ni hasa kukukumbusha utilie maanani maneno ya Mungu. Mungu asemapo: “Kwa masuala ya ndani ya roho, unapaswa kuwa makini kwa utaratibu; kwa maneno Yangu, unapaswa kuwa msikivu kwa makini. Unapaswa kulenga hali ambayo unaona Roho Yangu na nafsi Yangu ya mwili, maneno Yangu na nafsi Yangu ya mwili, kama kitu kimoja kizima kisichogawanyika, ili binadamu wote wataweza kuniridhisha mbele Yangu,” kwa kusoma maneno haya, binadamu, kwa mara nyingine, hupigwa bumbuazi. Walichoona jana kilikuwa neno la kuonya, ulikuwa mfano wa huruma ya Mungu, lakini leo mazungumzo yamegeuka ghafula kuwa mambo ndani ya roho—hili linamaanisha nini hasa? Kwa nini Mungu huendelea kubadilisha njia Yake ya kunena? Na mbona haya yote yanapaswa kuchukuliwa kama kitu kimoja kizima kisichogawanyika? Yawezekana kwamba maneno ya Mungu yanakosa uhalisi? Kwa kutafakari maneno haya, mtu hutambua hili: Wakati ambapo Roho wa Mungu na mwili vimetengana, basi mwili huo ni mwili wa maumbile ulio na sifa za mwili wa maumbile, kwa maneno mengine, kile ambacho watu huita maiti itembeayo. Mwili hutokana na Roho: Yeye ni kupata mwili kwa Roho, yaani, Neno lililopata mwili. Kwa maneno mengine, Mungu Mwenyewe huishi ndani ya mwili. Kutoka kwa hili mtu anaweza kuona mahali ambapo kuna kosa kubwa sana la kujaribu kutenganisha Roho na mwanadamu. Kwa sababu hii, ingawa Anaitwa “mwanadamu,” Yeye si wa jamii ya binadamu, na Hana sifa za binadamu: Huyu ni mtu ambaye Mungu hujivika, huyu ni mtu ambaye Mungu humthibitisha. Ndani ya maneno Roho wa Mungu amejumuishwa, na maneno ya Mungu yanafichuliwa moja kwa moja katika mwili. Hili linaeleza wazi zaidi kwamba Mungu huishi ndani ya mwili na ni Mungu wa vitendo zaidi, kutokana nalo inathibitishwa kwamba Mungu yupo, hivyo kumaliza enzi ya uasi wa binadamu dhidi ya Mungu. Kisha, baada ya kuufunza binadamu kuhusu njia inayoelekea kwa maarifa ya Mungu, Mungu anabadilisha mada tena, na kuchukua kipengele kingine cha tatizo.

“Nimetembea ulimwenguni kwa miguu Yangu, Nikinyoosha macho Yangu juu ya anga

yake nzima, na Nimetembea miongoni mwa wanadamu wote, Nikionja ladha tamu, ya asidi, chungu, na kali za uzoefu wa binadamu.” Kauli hii, ijapokuwa urahisi wake, siyo rahisi kufahamu. Ingawa mada imebadilika, kwa msingi inabaki ile ile: Bado inawawezesha binadamu kumjua katika mwili Wake. Kwa nini Mungu asema kwamba Ameenja ladha tamu, chachu, chungu, na kali za uzoefu wa binadamu? Mbona Asema kwamba Ametembea miongoni mwa wanadamu wote? Mungu ni Roho, lakini pia Yeye ni mwanadamu mwenye mwili. Roho, asiye fungwa na mipaka ya mwanadamu, Anaweza kukanyaga juu ya ulimwengu wote, Akiuzingira ulimwengu kwa tazamo la jumla. Kutoka kwa hili mtu anaweza kuona kwamba Roho wa Mungu hujaza eneo pana na wazi la ulimwengu na Hufunika dunia kutoka ncha hadi ncha; hakuna mahali ambapo hapajapangwa kwa mikono Yake, hakuna mahali pasipo na alama za nyayo Zake. Hata kama Roho, aliyepata mwili, anazaliwa kama mwanadamu, Yeye, kwa sababu ya kuweco Kwake kama Roho, Hakomi kuhitaji vitu vyote ambavyo wanadamu huhitaji, lakini kwa badala yake, kama mwanadamu wa kawaida, Hula chakula, Huvaa nguo, Hulala, na Huishi katika makazi, Akifanya kila kitu ambacho mwanadamu wa kawaida hufanya. Wakati huo huo, kiini cha ndani kikiwa tofauti, Yeye si sawa na kile ambacho mtu huzungumzia kwa kawaida kama mwanadamu. Ingawa Hustahimili mateso yote ya mwanadamu, Yeye kwa sababu hiyo Hatelekezi Roho; ingawa Hufurahia baraka, Yeye kwa sababu hiyo hasahau Roho. Roho na mwanadamu wameunganishwa kwa mapatano ya kimya; hao wawili Hawawezi kutenganishwa, na kamwe Hawajawahi kutenganishwa. Kwa kuwa mwanadamu ni kupata mwili kwa Roho, na hutoka kwa Roho, kutoka kwa Roho aliye na umbo, kwa hiyo Roho anayeishi ndani ya mwili si wa kupita uwezo wa binadamu, yaani, Hawezi kufanya mambo ya ajabu, ambalo ni kusema, Roho huyu hawezi kuondoka katika mwili wa maumbile, kwani Angefanya hivyo, kitendo cha Mungu cha kuwa mwili kingepoteza maana yake yote. Ni wakati ambapo Roho hudhihirishwa kwa ukamilifu ndani ya mwili wa maumbile tu ndipo binadamu wanaweza kusababishwa kumjua Mungu Mwenyewe wa vitendo, na wakati huo tu ndipo mapenzi ya Mungu hutimizwa. Ni baada tu ya Mungu kuwasilisha Roho na mwili mmoja mmoja kwa binadamu ndipo Huonyesha upofu na uasi wa mwanadamu: “lakini mwanadamu hakuwahi kweli kunitambua, wala hakuniona Nikitembea ng’ambo.” Kwa upande mmoja, Mungu asema kwamba, bila kujulikana kwa ulimwengu, Yeye hujificha ndani ya mwili, bila kufanya kamwe jambo lolote la miujiza kwa wanadamu kuona; kwa upande mwingine, Hulalamika dhidi ya binadamu kwa kukosa kumjua. Hakuna, hata hivyo, ukinzani ndani ya hili. Kwa kweli, ikitazamwa katika utondoti wake, si vigumu kuona kwamba kuna pande mbili kwa njia ambayo kwayo Mungu hutimiza malengo Yake. Sasa, kama Mungu angetekeleza ishara na maajabu ya miujiza, basi, bila kulazimika kuanza kazi yoyote kubwa, Angemlaani tu mtu kufa kwa kinywa Chake Mwenyewe, mtu huyo angekufa papo hapo, na kwa njia hii kila mwanadamu angeridhishwa; lakini hili halingetimiza lengo la Mungu katika kuwa mwili. Kama Mungu angefanya hili kweli, binadamu hawangeweza

kamwe, kwa akili zao za kufahamu, kuamini kuweco Kwake, haungeweza kamwe kuamini kweli, na zaidi ya hayo ungedhania kwamba shetani ni Mungu. Hata la muhimu zaidi, binadamu hawangejua tabia ya Mungu kamwe: Je, hiki si kipengele kimoja cha maana ya Mungu kuwa ndani ya mwili? Kama binadamu hawawezi kumjua Mungu, basi daima itakuwa Mungu asiye dhahiri, Mungu wa miujiza, ambaye Ana utawala mkubwa katika ufalme wa binadamu: Hili halingekuwa suala la fikira za mwanadamu kummiliki mwanadamu? Au, kulitamka hili tena kwa dhahiri zaidi, Shetani, ibilisi, hangukuwa ana utawala mkubwa? “Kwa nini Nasema Narejesha mamlaka Yangu? Kwa nini Nasema kwamba kupata mwili kuna maana nyingi sana?” Wakati ambapo Mungu hupata mwili, huo ndio wakati ambapo Hurejesha mamlaka Yake; pia ni wakati ambapo uungu Wake hujitokeza moja kwa moja kufanya kazi Yake. Hatua kwa hatua, kila mwanadamu huja kumjua Mungu wa vitendo, na kwa ajili ya hili nafasi inayoshikiliwa na Shetani ndani ya moyo wa mwanadamu hukandamizwa kabisa huku nafasi ya Mungu ikikuzwa. Awali, Mungu aliyekuwapo katika akili za watu alitambulika kama picha ya shetani, Mungu ambaye alikuwa hashikiki, Haonekani, na hata hivyo mtu aliamini Mungu huyu sio tu kuweco bali pia kuweza kutekeleza kila aina ya ishara na maajabu ya miujiza na kufichua kila aina ya mafumbo, kama vile kutisha kwa waliopagawa na pepo. Hili latosha kuthibitisha kwamba Mungu aliye ndani ya akili za watu si picha ya Mungu lakini badala yake ni picha ya kiumbe kando na Mungu. Mungu asema kwamba Anataka kuchukua nafasi inayomiliki asilimia 0.1 ya moyo wa mwanadamu, na kwamba hiki ni kiwango cha juu sana Atakacho kwa binadamu. Hakuna tu upande wa juujuu kwa kauli hii; pia kuna upande wa kweli. Kama haingefafanuliwa kwa njia hii, watu wangefikiria matakwa ambayo Mungu huhitaji kutoka kwao kuwa duni sana, kana kwamba Mungu alielewa kidogo sana kuwahusu. Je, hii siyo saikolojia ya binadamu?

Kama mtu atachukua yaliyo hapo juu na kuweka pamoja na mfano wa Petro ulio hapa chini, watapata kwamba Petro alikuwa kweli mtu aliyemjua Mungu bora zaidi, kwa sababu aliweza kuachana na Mungu asiye dhahiri na kufuatilia ufahamu wa Mungu wa vitendo. Kwa nini Mungu alitaja hoja maalum ya kufahamu kwamba wazazi wake walikuwa pepo waliompinga Mungu? Kutokana na hili inathibitishwa kwamba Petro hakuwa akimfuatilia Mungu aliye ndani ya moyo wake mwenyewe, na kwamba wazazi wake wanawakilisha Mungu asiye dhahiri: Hili ni kusudi la Mungu katika kuleta mfano wa wazazi wa Petro. Wengi sana wa watu huwa hawazingatii hasa ukweli huu, wakimakinikia uangalifu wao badala yake kwa maombi ya Petro, kwa kiwango ambacho wengine hata huweka maombi ya Petro daima ndani ya midomo yao na akilini mwao, lakini bila kamwe kufikiria kutofautisha Mungu asiye dhahiri na ufahamu wa Petro. Kwa nini Petro alienda kinyume cha wazazi wake na kutafuta kumjua Mungu? Kwa nini alichanganya mafunzo aliyokuwa amejifunza kutoka kwa wale waliokuwa wameshindwa zamani ili kujichochea kwa juhudi kuu zaidi? Kwa nini alisimilisha imani na upendo wa wale wote

waliokuwa wamempenda Mungu kote kote katika enzi? Petro alielewa kwamba kila kitu chema hutokana na Mungu—huja moja kwa moja kutoka kwa Mungu bila kupitia utengenezaji wowote na Shetani. Kutoka kwa hili mtu anaweza kuona kwamba Yule aliyemjua alikuwa Mungu wa vitendo na si Mungu wa miujiza. Kwa nini Mungu asema kwamba Petro alitilia maanani kwa njia maalum kusimilisha imani na upendo wa wale wote waliompenda Mungu kote kote katika enzi? Kutoka kwa hili mtu anaweza kuona kwamba sababu kuu mbona watu wameshindwa kote kote katika enzi ni kwamba walikuwa tu na imani na upendo lakini hawakumjua Mungu wa vitendo, na kwa hiyo imani yao iliendelea kuwa isiyo dhahiri. Kwa nini Mungu hutaja tu imani ya Ayubu mara nyingi bila kusema hata mara moja kwamba alimjua Mungu, na zaidi ya hayo kumwita wa chini kwa Petro? Kutoka kwa maneno ya Ayubu, “Nimesikia kukuhusu kwa kusikia na masikio: lakini sasa jicho langu lakuona,” mtu anaweza kuona kwamba Ayubu alikuwa tu na imani lakini bila ufahamu. Kwa kusoma kauli, “Na mfano usiofaa wa wazazi wake kuwa kama foili^[a], hii ilimwezesha kwa urahisi kutambua upendo na huruma Yangu,” watu wengi watachochewa kuleta maswali mengi: Ni kwa nini Petro anamjua Mungu tu anapowekwa dhidi ya mfano wa kinyume, lakini sio moja kwa moja? Ni kwa nini anajua tu huruma na upendo, lakini mambo mengine hayatajwi? Ni wakati tu ambapo mtu hutambua kutokuwa kweli kwa Mungu asiye dhahiri ndipo mtu hugeuka kuweza kufuatilia ufahamu wa Mungu wa vitendo. Lengo la tamko hili ni kuwaongoza watu kung’oa Mungu asiye dhahiri kutoka mioyoni mwao. Kama binadamu wangukuwa daima wamejua sura ya kweli ya Mungu, tangu mwanzoni mwa uumbaji kufikia siku ya leo, basi hawangukuwa wanaojua sana njia za Shetani, kama inavyojulikana kutoka kwa methali, “Mtu huwa hajali ardhi tambarare mpaka avuke mlima,” ambayo inaeleza wazi kwa utoshelevu maana ya Mungu katika kunena maneno haya. Kwa vile Angependa kuwaongoza watu kufahamu kwa kina zaidi ukweli wa mfano ambao Ametoa, Mungu anatia mkazo wa kusudi kwa huruma na upendo, Akithibitisha kwamba enzi ambayo Petro aliishi ndani ilikuwa Enzi ya Neema. Ikitazamwa kwa mtazamo mwingine, hii inafichua zaidi waziwazi sura ya kutisha ya shetani, ambaye hunasa mtegoni na kuwapotosha tu binadamu, na hivyo huanzisha, hata kwa utofauti mkavu zaidi, upendo na huruma ya Mungu.

Mungu pia anaeleza kwa muhtasari ukweli kuhusu majaribio ya Petro na zaidi ya hayo. Anaeleza hali zao halisi, ili watu waweze kutambua bora yafuatayo: kwamba Mungu hana huruma na upendo tu, lakini pia Ana uadhama na ghadhabu, na kwamba wanaoishi kwa amani sio lazima kwamba wanaishi katikati ya baraka za Mungu. Zaidi ya hayo, kuwaambia watu kuhusu uzoefu wa Petro baada ya majaribio yake kunaonyesha hata kwa dhahiri zaidi ukweli wa maneno haya ya Ayubu: “Tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” Hii inatosha kuonyesha kwamba Petro alikuwa amefikia ufahamu usio na kifani wa Mungu, kitu ambacho hakuna yeyote katika enzi yoyote iliyotangulia alikuwa amewahi kufikia:

Hiki ndicho Petro alipata wakati aliposimilisha imani na upendo wa wale wote ambao walikuwa wamempenda Mungu kote kote katika enzi na kuchanganya mafunzo ya kushindwa kwa zamani ili kujihimiza. Kwa sababu hii, yeyote ambaye hufikia ufahamu halisi wa Mungu huitwa “tunda,” na Petro ni mmoja miongoni mwa hawa. Katika maombi ya Petro kwa Mungu mtu anaweza kuona maarifa halisi ya Mungu ambayo alipata kupitia majaribio yake, lakini dosari moja ndogo ni kwamba hakuweza kufahamu kwa ukamilifu mapenzi ya Mungu. Hii ndiyo maana, kwa kujenga juu ya msingi wa maarifa ya Mungu ambayo Petro alipata, Mungu ameanzisha matakwa ya “kumiliki asilimia 0.1 pekee ya moyo wa mwanadamu.” Kwa kuzingatia ukweli kwamba hata Petro, mtu aliyemjua Mungu bora zaidi, hakuweza kuelewa mapenzi ya Mungu sawasawa, inaweza tu kuhitimishwa kwamba binadamu hawajaandaliwa hasa na chombo cha kumjua Mungu, kwa vile Shetani tayari amempotosha mwanadamu kwa kiasi hicho, na hili linawaongoza watu wote kujua kiini cha binadamu. Haya masharti ya mwanzo mawili—kwamba binadamu wanakosa chombo cha kumjua Mungu na zaidi ya hayo umepenywa na Shetani kabisa—yanatoa mandhari ya kuonyesha nguvu kuu za Mungu, kwa kuwa Mungu, kupitia tu utumiaji wa maneno na bila hata kulazimika kuanza aina yoyote ya kazi, amechukua nafasi fulani katika moyo wa mwanadamu. Kwa nini kufikia asilimia 0.1 kuna maana ya kufikia utimizaji wa mapenzi ya Mungu? Kulieleza hili kwa kuzingatia ukweli kwamba Mungu hakumpa mwanadamu chombo kinachozungumziwa: Ikiwa, wakati chombo hiki hakipo, binadamu wangepikia asilimia mia moja ya maarifa, basi kila hatua na kitendo cha Mungu vingekuwa kitabu kilicho wazi kwa mwanadamu, na, kwa ajili ya tabia ya asili ya mwanadamu, angemuasi Mungu mara moja, akiinuka kumpinga hadharani (hivi ndivyo alivyoanguka Shetani). Na kwa hiyo Mungu huwa hamdunishi mwanadamu kamwe. Hili ni kwa sababu tayari Amemchambua mwanadamu kabisa, kiasi kwamba Anajua kila kitu kwa ubayana ulio dhahiri kabisa hata mpaka kwa kiasi gani cha maji kimechanganywa na damu yake: Je, sembuse kuelewa kwa dhahiri zaidi asili ya mwanadamu ya kuonekana? Mungu hafanyi makosa kamwe, na zaidi ya hayo, katika kutoa matamshi Yake, Huchagua maneno Yake kwa usahihi mkubwa. Kwa sababu hii, ukweli kwamba Petro hakuwa sahihi katika kuelewa mapenzi ya Mungu haikanushi ukweli kwamba yeye pia ni mtu aliyemjua Mungu bora zaidi, na kilicho zaidi vitu hivi viwili havihusiani kabisa. Mungu hakuleta mfano wa Petro ili kulenga uangalifu wa watu kwake. Kwa nini Petro aliweza kufikia maarifa ya Mungu ikiwa hata mtu kama Ayubu hangeweza? Kwa nini angesema kwamba mtu anaweza kuyafikia na bado pia aseme kwamba ni kwa ajili ya nguvu kuu za Mungu? Je, ni kweli kwamba kipaji cha asili cha binadamu ni kizuri? Watu hawaoni ni rahisi kuelewa hoja hii—hakuna yeyote ambaye angejua maana yake ya ndani isipokuwa kama Ningeieleza. Lengo la maneno haya ni kuwawezesha wanadamu kufikia aina fulani ya mtazamo, ambayo kwayo watapata ujasiri kushirikiana na Mungu. Ni wakati huu tu ndiyo Mungu anaweza kufanya kazi kwa ushirika wa mwanadamu. Hivyo ndivyo hali ilivyo

katika eneo la kiroho, na haeleweki kabisa kwa mwanadamu. Ili kuondoa nafasi ya Shetani katika nyoyo za mwanadamu na kuipa Mungu nafasi hiyo badala yake-hii ndiyo inaamanisha kukataa mashambulizi ya Shetani, na hivyo basi inaweza kusemekana kwamba Kristo ameshuka hapa duniani, na hivyo huo tu inaweza kusemekana kwamba falme za duniani zimekuwa ufalme wa Kristo.

Inatajwa hapa kwamba Petro amekuwa sampuli na mwenye kuonyesha mtindo kwa wanadamu kwa maelfu ya miaka. Hili silo tu kwa ajili ya kufafanua ukweli kwamba yeye ni sampuli na kielelezo: Maneno haya ni mfano wa onyesho halisi la vita katika ulimwengu wa kiroho. Wakati huu wote Shetani amekuwa akimfinyanga mwanadamu, akiwa na matumaini yasiyofaa ya kuwameza binadamu na kisha kusababisha Mungu kuuharibu ulimwengu na kupoteza ushahidi Wake. Lakini Mungu alisema: “Kwanza Nitaumba mfano ili Niweze kuchukua nafasi ndogo kabisa ndani ya moyo wa mwanadamu. Katika hatua hii, binadamu hawanifurahishi wala kunijua kwa ukamilifu; hata hivyo, kwa kutegemea nguvu Zangu kuu, mwanadamu ataweza kunitii Mimi kabisa na kukoma kuniasi, na Nitatumia mfano huu kumtiisha Shetani, huku ni kusema, Nitatumia nafasi Yangu iliyo na asilimia 0.1 kuzuia nguvu zote ambazo Shetani amekuwa akitumia kumtawala mwanadamu.” Na kwa hiyo, leo, Mungu ametoa mfano wa Petro ili aweze kutumika kwa wanadamu wote kama sampuli ya kufuata. Kuyaweka haya pamoja na maneno ya mwanzo, mtu anaweza kuona ukweli wa kile alichosema Mungu kuhusu hali halisi katika ulimwengu wa kiroho: “Mambo hayako sasa kama yalivyokuwa wakati mmoja: Naenda kufanya mambo ambayo, tangu mwanzo wa uumbaji, dunia haijawahi kuyaona, Naenda kusema Maneno ambayo, kupitia enzi nyingi, wanadamu hawajawahi kuyasikia, kwa sababu Nauliza kwamba binadamu wote waje wanijue katika mwili.” Kutokana na hili mtu anaweza kuona, kile alichonena Mungu kukihusu Amekianza leo. Wanadamu wanaweza tu kuyaona mambo yanavyoonekana nje na sio hali halisi ndani ya ulimwengu wa kiroho. Kwa sababu hii, Mungu alisema kwa njia ya moja kwa moja na waziwazi: “Hizi ndizo hatua kwa usimamizi Wangu, ambazo binadamu hawazijui hata kidogo. Hata Ninapozizungumzia wazi, mwanadamu bado amechanganyikiwa sana kwa akili yake mpaka haiwezekani kumwelezea kila kitu kuzihusu. Kutoka hapa kuna unyenyekevu dhalili wa mwanadamu, sivyo?” Kuna maneno yasiyosemeka ndani ya maneno haya, yakieleza kwamba vita vimefanyika katika ulimwengu wa kiroho, kama ilivyodokezwa hapo juu.

Makusudi ya Mungu hayafanikishwi baada ya maelezo kwa ufupi kuhusu hadithi ya Petro, kwa hivyo Mungu anafanya matakwa yafuatayo kwa mwanadamu kuhusu mambo ya Petro: “Kote ulimwenguni na maeneo yasiyo na kikomo ya anga, kati ya vyote vinavyopatikana mbinguni kama ilvyo duniani, vitu vyote lukuki duniani, na mambo lukuki mbinguni yote yanatoa juhudi zote kwa ajili ya ukamilisho wa kazi Yangu. Hakika hamtamani kubakia tu kama

watazamaji walio kando, ambao huendeshwa hapa na pale na nguvu za Shetani?” Watu wameangaziwa sana baada ya kusoma kuhusu maarifa ya Petro, na ili kuwa hata mwenye ufanisi zaidi, Mungu huwaruhusu binadamu waone matokeo ya kutozuiliwa kwa utukutu na kutomjua Yeye, na zaidi ya hayo Anawaambia binadamu—mara nyingine tena na kwa usahihi mkuu zaidi—kuhusu hali halisi za vita katika ulimwengu wa kiroho. Ni kwa njia hii pekee ndio wanadamu wanaweza kuwa na tahadhari zaidi katika kujilinda dhidi ya kukamatwa na Shetani; zaidi ya hayo, inaeleza wazi kwamba, wakati huu, wakianguka, hawatapokea wokovu kutoka kwa Mungu tena kama walivyofanya wakati huu. Yakichukuliwa pamoja, maonyo haya kadhaa, katika kuzidisha fikira za binadamu kuhusu maneno ya Mungu, yamewasababisha watu kutunza huruma Yake kwa upendo zaidi na kushikilia kwa makini zaidi maneno Yake ya kuonya, hivyo kufikia kweli lengo la Mungu la kuwaokoa wanadamu.

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Kuhusu Maisha ya Petro

Petro ni mfano ambao Mungu aliutambulisha kwa wanadamu, na yeye ni mtu mashuhuri anayejulikana vizuri. Kwa nini mtu mnyonge kama huyo aliwekwa mahala kama mfano na Mungu na amesifiwa na vizazi vya baadaye? Bila shaka, ni wazi kwamba hili halitenganishwi na maonyesho yake na azimio lake la upendo kwa Mungu. Kuhusu wapi ambapo moyo wa Petro wa upendo kwa Mungu ulionyeshwa na kile ambacho uzoefu wake wa maishani ulivyokuwa kwa kweli, lazima turudi kwa Enzi ya Neema kutazama tena desturi za wakati huo, ili kumwona Petro wa enzi hiyo.

Petro alizaliwa katika nyumba ya kawaida ya wakulima wa Kiyahudi. Wazazi wake waliikimu familia yote kwa kufanya ukulima, naye alikuwa mzaliwa wa kwanza kati ya watoto wote; alikuwa na ndugu wanne. Bila shaka hii siyo sehemu muhimu ya hadithi ya kusimulia—Petro ni mhusika wetu mkuu tu. Alipokuwa na umri wa miaka mitano, wazazi wake walianza kumfunza kusoma. Wakati huo Wayahudi walikuwa wenye maarifa kabisa—walikuwa walioendelea sana katika mawanda kama vile kilimo, viwanda, na biashara. Chini ya athari ya aina hiyo ya mazingira ya kijamii, wazazi wote wawili wa Petro walikuwa wamepata elimu ya juu zaidi. Hata ingawa walitoka mashambani, walikuwa na jumla ya maarifa mengi kabisa, ikifananishwa na mwanafunzi wa kawaida wa chuo kikuu wa leo. Ni wazi kwamba kuzaliwa katika hali bora sana za kijamii kama hizo ilikuwa bahati nzuri ya Petro. Alikuwa mwenye akili sana na alielewa mambo mapya kwa urahisi. Baada ya yeye kuanza shule, katika masomo yake aliweza kufanya uamuzi kutoka kwa vitu vingine bila kuonekana kutumia juhudi zozote. Wazazi wake walijivunia kuwa na mwana stadi kama huyo, kwa hiyo walifanya kila juhudi kumkubalia

kwenda shuleni, wakitumaini kwamba angefaulu, na angeweza kupata aina fulani ya cheo cha urasimu katika jamii ya wakati huo. Bila kutambua, Petro alikuza moyo wa kupenda kumjua Mungu, kwa hiyo alipokuwa na umri wa miaka kumi na minne na katika shule ya upili, alichoshwa na mtalaa wa Tamaduni za Wagiriki za Kale alizokuwa akijifunza, na hasa aliwadharau watu na vitu vya kubuni katika historia ya Kigiriki ya kale. Kuanzia wakati huo na kuendelea, Petro, ambaye alikuwa ameingia tu katika uchipukizi wa ujana wake, alianza kuchunguza maisha ya binadamu na kuwasiliana na jamii. Hakulipiza kujitahidi sana kwa wazazi wake na dhamiri kwa sababu aliona kwa dhahiri kwamba watu wote walikuwa wakiishi katika kipindi cha kujidanganya, na wote walikuwa wakiishi katika maisha yasiyo na maana, wakiharibu maisha yao wenyewe kwa ajili ya kushindania umaarufu na mali. Sababu iliyomchochea kuona hili ilihusiana hasa na mazingira ya kijamii aliyokuwa ndani. Kadri ambavyo watu wanakuwa na maarifa, ndivyo mahusiano ya kati ya watu wawili yanavyokuwa magumu zaidi kufahamika, na kadri ambavyo dunia za ndani za watu zinavyokuwa ngumu zaidi kufahamika, ndivyo panavyokuwa tupu zaidi mahali ambapo pana watu. Chini ya hali hizi, Petro alianza kutafuta habari kila mahali wakati wake wa ziada, na watu wa dini walikuwa katika idadi ya wengi wa wale aliotafuta habari kutoka kwao. Ilionekana kwamba alikuwa na hisia isiyo dhahiri moyoni mwake kwamba mambo yote yasiyotambulikana katika ulimwengu wa binadamu yangebainishwa katika ulimwengu wa dini, kwa hiyo alienda mara kwa mara katika sinagogi iliyokuwa karibu na nyumbani kwake ili kuhudhuria ibada ya kuabudu. Wazazi wake hawakujua kuhusu jambo hili, na kabla ya muda mrefu Petro, ambaye kila mara alikuwa na mwenendo na taaluma bora sana, alianza kuchukia kwenda shuleni. Chini ya uangalizi wa wazazi wake alimaliza shule ya upili kwa shida. Aliogelea hadi pwani kutoka katika bahari ya maarifa, akavuta pumzi kabisa, na tangu wakati huo na kuendelea hakuna aliyemfunza au kumwekea mipaka.

Baada ya yeye kumaliza shule alianza kusoma kila aina ya vitabu, lakini alipokuwa na umri wa miaka kumi na saba, bado alikosa uzoefu wa jamii. Baada ya kuhitimu na kuondoka shuleni, alijiruzuku kwa ukulima huku pia akitenga muda mwingi alivyoweza kusoma vitabu na kuhudhuria ibada za kuabudu za dini. Wazazi wake, ambao walijawa na tumaini kwake mara kwa mara waliilaani Mbinguni kuhusu “mtoto mwasi” huyu. Lakini licha ya hili, moyo wake ambao ulikuwa na njaa na kiu ya haki haungekomeshwa. Alipitia vipingamizi si haba katika uzoefu wake, lakini alikuwa na moyo wenye uroho, kwa hiyo alichipuka kama nyasi baada ya mvua kunyesha. Kabla ya muda mrefu “alibahatika” kukutana na watu wa kiwango cha juu katika ulimwengu wa dini, na kwa sababu moyo wake wa kuwa na hamu ulikuwa thabiti sana, aliwasiliana na watu hao zaidi na zaidi kwa kawaida na alitumia karibu muda wake wote miongoni mwao. Wakati ambapo alikuwa tu amezamishwa ndani ya furaha ya kuridhika kwake,

aligundua ghafula kwamba miongoni mwa watu hao, wengi wao walikuwa na imani kwa maneno tu lakini hakuna kati yao aliyejitolea katika moyo wake. Na moyo wake mwadilifu, wa kweli, Petro angeweza kuhimili pigo kama hilo? Aligundua kwamba karibu watu wote ambao aliwashughulikia walikuwa wanyama ndani ya mavazi ya binadamu—walikuwa wanyama wenye sura za binadamu. Wakati huo Petro alikuwa mnyofu sana, kwa hiyo mara nyingi aliwasihi kwa yakini, lakini ni vipi ambavyo watu wa dini wa hila, wajanja wangeweza kusikiliza kusihi kwa kijana aliyejawa na nguvu na bidii? Ni wakati huo ndipo Petro alihisi utupu wa maisha ya binadamu, na alipochukua hatua yake ya kwanza kuelekea katika hatua ya maisha, alishindwa.... Mwaka mmoja baadaye, alihama kutoka kwenye sinagogi na akaanza maisha yake ya kujitawala mwenyewe.

Baada ya Petro mwenye umri wa miaka 18 kupitia kipingamizi kimoja, alikuwa mkomavu na mstaarabu zaidi. Usungu wake wote wa ujana ulitoweka tu, na maasumu ya ujana na kutokuwa na hila alikuwa nako kulizimwa bila huruma na kipingamizi hicho. Tangu wakati huo na kuendelea akaanza maisha kama mvuvi. Baada ya hilo, mtu angeweza kuona kwamba kulikuwa na watu juu ya mashua yake ya kuvua waliokuwa wakisikiliza alichokuwa akihubiri; alikuwa akivua ili kupata riziki na kuhubiri kotekote mahali hapo. Kila mtu aliyemhubiria alifadhaishwa na mahubiri yake kwa sababu alichozungumzia kilikubaliana sana na mioyo ya watu wa kawaida wakati huo. Watu wote walivutwa sana na uaminifu wake, na aliwafunza watu mara kwa mara kuwashughulikia wengine kwa yakini na kumwita Bwana wa mbingu na dunia na vitu vyote ndani ya kila kitu, na kutopuza dhamiri zao na kufanya yale mambo yasiyo ya kupendeza, bali kumridhisha Mungu wanayempenda mioyoni mwao katika mambo yote.... Watu walivutwa sana mara kwa mara baada ya kusikiliza mahubiri yake. Wote walitiwa moyo naye na wangetokwa na machozi kwa uchungu mara kwa mara. Wakati huo, kila mtu aliyemfuata alikuwa na uvutiwaji sana naye. Wote walikuwa fukara, na kwa sababu ya athari za kijamii wakati huo, bila shaka alikuwa na wafuasi wachache; alikuwa pia mwenye kupatwa na mateso mara kwa mara kutoka kwa ulimwengu wa dini katika jamii ya wakati huo. Kwa sababu hii alikuwa akizunguka kote siku zote, na aliishi maisha ya upweke kwa miaka miwili. Alipata ujuzi mwingi sana katika miaka miwili hiyo ya matukio yasiyo ya kawaida, na alijifunza kiasi kikubwa sana cha mambo ambayo hakuwa ameyajua awali. Petro wakati huo alikuwa mtu tofauti kabisa na yule aliyekuwa katika umri wa miaka 14—ilionekana hawakuwa na chochote sawa. Katika miaka hiyo miwili alikutana na kila aina ya watu na aliona kila aina ya ukweli kuhusu jamii; tangu wakati huo na kuendelea alijiondoa polepole na kila aina ya kaida za dini kutoka kwa ulimwengu wa dini. Kwa sababu ya mwelekeo katika kazi ya Roho Mtakatifu wakati huo, aliathiriwa kabisa. Wakati huo Yesu pia alikuwa amefanya kazi kwa miaka kadhaa, kwa hiyo kazi yake pia iliathiriwa na kazi ya Roho Mtakatifu wakati huo, hata hivyo, bado hakuwa

amekutana na Yesu. Kwa sababu hiyo, wakati ambapo alikuwa akihubiri, alipata vitu vingi ambavyo vizazi vya watakatifu havikuwa vimepata kamwe. Bila shaka, wakati huo alikuwa anafahamu kwa uchache kuhusu Yesu lakini hakuwa kamwe amepata nafasi ya kukutana na Yeye ana kwa ana. Alitumaini tu na kuwa na kiu ndani ya moyo wake ya kumwona mtu huyo wa mbinguni aliyezaliwa kwa Roho Mtakatifu.

Alikuwa anavua juu ya mashua yake wakati wa utusiutusi jioni moja (karibu na pwani ya Bahari ya Galilaya iliyotajwa wakati huo), na ingawa alikuwa na ufito wa kuvua mikononi mwake, alikuwa na mambo mengine katika mawazo yake. Nuru ya magharibi ilianguka juu ya maji kama dimbwi la damu ndani ya eneo pana na wazi la bahari. Nuru iliakisi juu ya uso mchanga wa Petro, tena mtulivu na thabiti, kana kwamba alikuwa amezama katika mawazo. Wakati huo upepo mwanana ulijitokeza, na akahisi papo hapo kwamba maisha yake yalikuwa ya ukiwa, na hivyo ghafla alipitia hisia ya huzuni. Maji ndani ya bahari yaliakisi nuru hiyo wimbi baada ya wimbi, na ilikuwa wazi kwamba hakuwa na moyo wa kuvua. Wakati ule ule alipokuwa amezama ndani ya mawazo ya kila aina ya mambo, ghafla alimsikia mtu nyuma yake akisema: “Simoni Myahudi, mwana wa Yona, siku za maisha yako ni za ukiwa. Je, utanifuata?” Petro aliposikia haya alipigwa na butwaa, na akaanguka ufito wa kuvua uliokuwa mikononi mwake, na punde ukazama chini ya maji. Petro alikurupuka kugeuka pande zote, na akamwona mtu amesimama ndani ya mashua yake. Alimtazama Yeye toka juu hadi chini: nywele Zake, zilining’inia juu ya mabega Yake, zilikuwa manjano kama dhahabu kidogo katika nuru ya jua na nguo Zake zilikuwa za rangi ya kijivu. Alikuwa wa kimo cha wastani na mavazi Yake yalikuwa ya mwanamume wa Kiyahudi kabisa. Katika nuru ya utusiutusi, nguo Zake za rangi ya kijivu zilionekana nyeusi kidogo, na uso Wake ulionekana kuwa na mng’ao kidogo. Petro alijitahidi kumwona Yesu mara nyingi lakini kila wakati hakuweza kufanya hivyo. Wakati huo aliamini ndani ya Roho yake kwamba mtu huyo bila shaka alikuwa Yule mtakatifu wa moyo wake, kwa hiyo alisujudu katika mashua yake: “Yaweza kuwa Wewe ni Bwana ambaye amekuja kuhubiri injili ya ufalme wa mbinguni? Nimesikia kuhusu matukio Yako lakini sijawahi kukuona Wewe. Nimekuwa nikitaka kukufuata Wewe, lakini singekupata Wewe.” Yesu alikuwa tayari ametembea hadi kwa sehemu ya kuwekea mizigo ya mashua yake na Alikuwa Ameketi chini kwa utulivu. Akasema:^[a] “Simama na uketi karibu na Mimi. Nimekuja kuwatafuta wale wanipendao Mimi kweli, na kueneza injili ya ufalme wa mbinguni. Naenda kila mahali kuwatafuta wale ambao ni wenye moyo mmoja na Mimi. Je, uko radhi?” Petro akajibu: “Lazima nimfuate yule ambaye ametumwa na Baba wa mbinguni. Lazima nimkubali yule ambaye ameteuliwa na Roho Mtakatifu. Kwa vile nampenda Baba wa mbinguni, ningewezaje kukosa kuwa radhi kufuata?” Ingawa dhana za dini ndani ya maneno ya Petro zilikuwa thabiti sana, Yesu alitabasamu na kuashiria kwa kichwa Chake kwa ridhaa. Wakati huo, hisia ya upendo wa

baba kwa Petro ilikua ndani Yake.

Petro alimfuata Yesu kwa miaka kadhaa na aliona mambo mengi ndani ya Yesu ambayo watu hawana. Baada ya kumfuata Yeye kwa mwaka mmoja, aliteuliwa na Yesu kama mkuu wa wanafunzi kumi na wawili. (Bila shaka hili lilikuwa jambo la moyo wa Yesu, na watu hawakuweza kabisa kuliona.) Kila kitendo cha Yesu kilikuwa mfano kwake katika maisha yake, na mahubiri ya Yesu yaliwekwa hasa katika kumbukumbu ndani ya moyo wake. Alikuwa mwenye busara sana na wa kujitolea kwa Yesu, na kamwe hakuwa na malalamiko kumhusu Yesu. Hii ndiyo maana alikuwa mwandani mwaminifu wa Yesu popote Alipoenda. Petro alichunguza mafunzo ya Yesu, maneno Yake yasiyo makali, na kile Alichokula, Alichovaa, maisha Yake ya kila siku, na safari Zake. Alifuata mfano wa Yesu katika kila njia. Hakuwa wa kujidai, lakini alitupa vitu vyake yote vya awali vilivyopitwa na wakati akafuata mfano wa Yesu katika maneno na matendo. Ni wakati huo ndipo alihisi kwamba mbingu na dunia na vitu vyote vilikuwa ndani ya mikono ya Mwenyezi, na kwa sababu hii hakuwa na chaguo lake mwenyewe, lakini alichukua kila kitu ambacho Yesu alikuwa ili kiwe mfano wake. Angeweza kuona kutoka kwa maisha yake kwamba Yesu hakuwa wa kujivuna katika kile Alichofanya, wala Hakujigamba kuhusu Mwenyewe, lakini badala yake, Aliwavuta watu na upendo. Katika hali mbalimbali Petro angeweza kuona kile ambacho Yesu alikuwa. Hiyo ndiyo maana kila kitu ndani ya Yesu kilikuwa chombo ambacho Petro alikifuata kama mfano. Katika uzoefu wake, alihisi kupendeza kwa Yesu zaidi na zaidi. Alisema kitu kama hiki: “Nilimtafuta Mwenyezi katika ulimwengu na nikaona maajabu ya mbingu na dunia na vitu vyote, na hivyo nilikuwa na hisi kuu ya kupendeza kwa Mwenyezi. Lakini sikuwa kamwe na upendo halisi ndani ya moyo wangu, na sikuona kamwe kupendeza kwa Mwenyezi kwa macho yangu mwenyewe. Leo, katika macho ya Mwenyezi, nimetazamwa na fadhila na Yeye na hatimaye nimehisi kupendeza kwa Mungu, na hatimaye nimegundua kwamba kwa Mungu, siyo tu kuumba vitu vyote ambavyo vingewafanya wanadamu wampende Yeye. Katika maisha yangu ya kila siku nimepata kupendeza Kwake kusiko na kikomo; ni vipi ambavyo ingewezekana kuwekewa mipaka tu katika hali hii leo?” Muda ulipopita, vitu vingi vya kupendeza vilipatikana pia ndani ya Petro. Alikuwa mtiifu sana kwa Yesu, na bila shaka alipitia hasa vipingamizi vingi kwa kiasi fulani. Wakati ambapo Yesu alimpeleka katika sehemu mbalimbali kuhubiri, yeye alijinyenyekeza kila mara na kuyasikiliza mahubiri ya Yesu. Hakuwa kamwe mwenye kiburi kwa sababu ya miaka yake ya kufuata. Baada ya Yesu kumwambia kwamba sababu ya Yeye kuja ilikuwa kusulubiwa ili kuimaliza kazi Yake, alikuwa na huzuni sana mara kwa mara na angetokwa na machozi akiwa pekee yake kisiri. Hata hivyo, siku ile “ya kusikitisha” ilifika. Baada ya Yesu kushikwa, Petro alitokwa na machozi pekee yake juu ya mashua yake ya kuvua na akaomba kiasi kikubwa kuhusu jambo hili, lakini ndani ya moyo wake alijua kwamba yalikuwa mapenzi ya Mungu Baba

na hakuna ambaye angeyabadilisha. Yeye alikuwa akihuzunika na kutokwa na machozi siku zote kwa sababu ya athari ya upendo—bila shaka, huu ni udhaifu wa binadamu, kwa hiyo wakati ambapo alijua kwamba Yesu angepigiliwa misumari msalabani, alimuuliza Yesu: “Baada ya Wewe kuondoka Utarudi kuwa miongoni mwetu na kutuchunguza? Je, bado tutaweza kukuona Wewe?” Ingawa maneno haya yalikuwa manyofu kabisa, na pia yalikuwa yamejawa na fikira za binadamu, Yesu alijua ladha ya mateso ya Petro, kwa hiyo kupitia upendo Wake alikuwa mwenye huruma kuhusu udhaifu wake: “Petro, Nimekupenda wewe. Je, wajua hilo? Ingawa hakuna maana katika kile usemacho, Baba ameahidi kwamba baada ya kufufuka Kwangu, Nitaonekana kwa wanadamu kwa siku 40. Je, huamini kwamba Roho Wangu atawapa ninyi nyote neema mara kwa mara?” Baada ya hilo Petro alikuwa na faraja kiasi kidogo, lakini alihisi kila mara kulikuwa na kipingamizi katika kile ambacho kilikuwa kamili kwa upande mwingine. Kwa hiyo, baada ya Yesu kufufuliwa, Alionekana kwake wazi kwa mara ya kwanza, lakini ili kumzuia Petro kuendelea kushikilia fikira zake, Yesu alikataa chakula kingi mno ambacho Petro alikuwa amemwandalia Yeye na akatoweka kufumba na kufumbua macho. Wakati huo Petro hatimaye alikuwa na ufahamu wa kina kuhusu Yesu, na akampenda Bwana Yesu hata zaidi. Baada ya kufufuka Kwake, Yesu alimwonekana Petro mara kwa mara. Baada ya siku 40 wakati ambapo Alipaa mbinguni, Alimwonekana Petro mara tatu. Kila wakati ambapo Yeye alionekana ulikuwa wakati ambao kazi ya Roho Mtakatifu ilikuwa karibu kukamilishwa na kazi mpya ilikuwa karibu kuanzwa.

Petro alipata riziki kwa kuvua kotekote katika maisha yake yote, lakini hata zaidi, aliishi kwa ajili ya kuhubiri. Katika miaka yake ya baadaye, aliandika waraka wa kwanza na wa pili wa Petro, na aliandika barua kadhaa kwa kanisa la Filadelfia la wakati huo. Watu wakati huo walivutwa sana na yeye. Hakuwahubiria watu kamwe kwa kutegemea sifa zake mwenyewe, bali aliwapa ruzuku ya kufaa ya uzima. Katika maisha yake, hakisahau kamwe mafunzo ya Yesu wakati wa maisha Yake—alisalia kutiwa moyo. Wakati ambapo alikuwa akimfuata Yesu aliamua kuulipiza upendo wa Bwana kwa kifo chake na kwamba angefuata mfano wa Yesu katika vitu vyote. Yesu alimuahidi hili, kwa hiyo wakati ambapo alikuwa na umri wa miaka 53 (zaidi ya miaka 20 baada ya kuachana na Yesu), Yesu alionekana kwake kutambua azimio lake. Katika miaka saba ya kufuata jambo hilo, Petro alitumia maisha yake katika kujijua. Siku moja, mwisho wa miaka hii saba, alisulubiwa juu chini, kukakomesha maisha yake yasiyo ya kawaida.

Tanbihi:

a. Maandishi ya asili hayana neno “Akasema.”

Sura ya 8

Mungu anenapo neno Lake kutokana na mtazamo wa Roho, sauti Yake huelekezwa kwa

wanadamu wote. Mungu anenapo neno Lake kutokana na mtazamo wa mwanadamu, sauti Yake huelekezwa kwa wote wafuatao uongozi wa Roho Wake. Mungu anenapo neno Lake kutokana na mtazamo wa nafsi ya tatu (kile ambacho watu hutaja kama mtazamaji), Anaonyesha neno Lake moja kwa moja kwa watu ili watu wamwone kama mtoa maoni, na huonekana kwamba kutoka kinywani Mwake hutoka mambo yasiyo na kikomo ambayo mwanadamu hayajui, mambo ambayo mwanadamu hawezi kuelewa. Je, hilo si sahihi? Mungu anenapo neno Lake kutokana na mtazamo wa Roho hilo huwashangaza binadamu wote. “Upendo wa mwanadamu Kwangu ni mdogo mno na imani yake Kwangu ni ndogo ajabu. Kama sehemu kubwa ya maneno Yangu haingeelekezwa kwa udhaifu wa mwanadamu, angejigamba na kutia mambo chumvi, na angehubiri na kubuni nadharia zenye kuvutia, ni kama aliye na maarifa yote na anayejua yote kuhusu masuala duniani.” Maneno haya hayafichui tu tabia halisi ya mtu na kufichua nafasi ya Mungu ndani ya mioyo ya watu, bali pia hufichua maisha yote ya wanadamu. Kila mtu huamini kwamba yeye ni wa ajabu na hata hajui kwa kweli kuna neno linaloitwa “Mungu” kwa hiyo yeye hubuni nadharia nyingi za kuvutia. Hata hivyo, huku “kubuni nadharia nyingi za kuvutia” si “kunena” kwa hali ambayo watu wanaielewa. Badala yake, ina maana kwamba binadamu wamepotoshwa na Shetani kiasi kwamba kila kitu wafanyacho humkaidi Mungu na humpinga Mungu wazi, na kwamba kiini hasa cha kile mwanadamu hufanya hutoka kwa Shetani na kiko katika upinzani kwa Mungu, ni kitendo cha kujitegemea, na huenda kinyume na mapenzi ya Mungu. Hii ndiyo maana Mungu husema kwamba watu wote hubuni nadharia nyingi za kuvutia. Kwa nini Mungu asema kwamba sehemu kubwa ya maneno Yake huelekezwa kwa udhaifu wa mwanadamu? Kwa sababu kwa mujibu wa kusudi la Mungu, kama Hangefichua mambo yaliyofichwa katika ulimwengu wa ndani wa moyo wa mwanadamu, basi hakuna mtu ambaye angetii, na kwa hivyo hangejielewa, na hangemcha Mungu. Hii ni kusema kwamba makusudi ya mwanadamu yasipofichuliwa, basi mwanadamu atathubutu kufanya chochote, labda hata kuelekeza laana kwa Mbingu au kwa Mungu. Huu ni udhaifu binadamu. Hivyo basi Mungu ananena hivi: “Nasafiri hadi katika pembe zote za ulimwengu katika hali ya kutafuta kwa kudumu wale wanaolingana na nia Yangu na wanaostahili kwa matumizi Yangu.” Kauli hii, ikiunganishwa na kile kinachosemwa baadaye kuhusu maamkizi ya ufalme yanayovuma kwa urasmi, inatumika kuonyesha kwamba Roho wa Mungu anajishughulisha na kazi mpya duniani; ni kwamba tu wanadamu hawawezi kuona kwa macho yao ya kimwili. Kwa vile inasemwa kwamba Roho yuko duniani Akifanya kazi mpya, ulimwengu wote pia hupitia mabadiliko ya maana sana: Wana wa Mungu na watu wa Mungu hawaanzi tu kukubali ushuhudiaji wa kupata mwili kwa Mungu, zaidi ya hayo, kila dini, kila dhehebu, kila tabaka, na kila mahali, kwa viwango mbalimbali, huukubali pia. Ni badiliko kubwa la ulimwengu katika ulimwengu wa kiroho. Huo hutetemesha ulimwengu wote wa dini kabisa, ambalo ni sehemu ya maana ya “zilizala” iliyotajwa zamani. Inayofuata, malaika wanaanza kazi yao rasmi na Waisraeli

wanarudi katika nchi yao ya asili, wasiwahi kupotea tena, na wale wote waliojumuishwa huanza kukubali uchungaji. Kinyume, Wamisri wanaanza kujitoa kwa eneo la wokovu Wangu, yaani, kupokea kuadibu Kwangu (lakini hilo bado halianzi kwa urasmi). Kwa hiyo ni katika wakati huu wa mabadiliko haya makubwa ya kutokea wakati mmoja duniani ndio maamkizi ya ufalme yanavuma kwa urasmi, Hiki ndicho watu wameita, “wakati ambapo Roho aliyeongezwa nguvu mara saba Huanza kufanya kazi.” Kila wakati ambapo Mungu hufanya kazi ya kupata tena, katika awamu hizi (au katika nyakati hizi za mpito), hakuna anayeweza kuhisi kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa hivyo, maneno ya Mungu kwamba “Mwanadamu anapokata tamaa” huonekana kuwa kweli. Aidha, katika kila awamu hizi za mpito wakati ambapo wanadamu hukata tamaa, au wanapohisi mkondo huu si sahihi, Mungu huanza upya na huchukua hatua inayofuata ya kazi Yake. Tangu wakati wa uumbaji mpaka sasa, Mungu kufanya kazi ya kupata tena na kubadilisha mbinu ambazo Yeye hufanyia kazi kunafanana kwa njia hii. Ingawaje watu wengi zaidi, kwa viwango tofautitofauti, wanaweza kuelewa vipengele vyake vingine, mwishowe hata hivyo wao huondolewa kwa mbubujiko wa maji kwa sababu kimo chao ni kidogo sana; hawawezi kuelewa hatua za kazi ya Mungu na hivyo wao huondolewa. Hata hivyo, hii pia ni mbinu ya Mungu ya kuwatakaswa watu, na hii ni hukumu ya Mungu kwa fikira za zamani za wanadamu. Kadri watu wanavyokuwa na msingi zaidi, ndivyo fikira zao za kidini kuhusu Mungu huwa kubwa zaidi, ambazo ni ngumu wao kuzipuuzwa; wao hushikilia mambo ya zamani na ni vigumu wao kukubali nuru mpya. Kwa upande mwingine, kama mtu anasimama, mtu lazima awe na msingi fulani, lakini watu wengi sana huwa na tatizo la kuweka kando fikira zao. Hii ni kweli hasa kwa fikira zao kuhusu Mungu mwenye mwili wa leo, ambalo ni wazi na rahisi kuona.

Katika tamko la siku hii, Mungu alizungumza mengi kuhusu maono, na hakuna haja ya kueleza kinaga ubaga. Mungu anazungumza kimsingi kuhusu jinsi ujenzi wa kanisa unaweka msingi wa ujenzi wa ufalme. Hasa, wakati kanisa lilikuwa likijengwa, lengo kuu lilikuwa kuwashawishi watu moyoni na kwa neno, ingawa hawajamjua Mungu mwenye mwili kwa macho yao wenyewe. Ingawaje walikuwa na imani ndani ya mioyo yao, hawakumjua Mungu mwenye mwili kwa sababu katika hatua hiyo Hangetofautishika na mtu. Katika Enzi ya Ufalme, wote lazima waonyeshe kusadiki sana ndani ya mioyo yao, kunena kwao, na macho yao. Kutoka hapa, ni wazi kwamba ili wote waonyeshe kusadiki sana ndani ya mioyo yao, kunena kwao, na macho yao, lazima waruhusiwe kumjua Mungu aishiye katika mwili kwa macho yao ya mwili. Hili haliwezi kufanikishwa katika hali ambayo watu wanalazimishwa kufanya jambo kwa sababu hawana hiari nyingine au ambayo watu wana imani isiyo ya kudumu. Badala yake, watu wataridhishwa moyoni na kwa neno kupitia ufahamu. Kwa hivyo, katika hatua hii ya ujenzi hakuna kupiga au kuua. Badala yake, inawaruhusu watu kupata nuru kupitia neno la Mungu, na kupitia hili waweze kufuatilia na kuchunguza ili kwa kufichika akilini watakuja kumjua Mungu

mwenye mwili. Kwa hiyo kumhusu Mungu, hatua hii ya kazi ni rahisi zaidi, huacha maisha yaendeleo katika hali yake ya asili na haiendi kinyume na wanadamu. Hiyo, mwishowe, itamruhusu mwanadamu kuja kumjua Mungu kwa kawaida, kwa hiyo usiwe mwenye wahaka au kuwa na wasiwasi. Mungu aliposema, “vita vya ulimwengu wa kiroho vimewekwa wazi miongoni mwa watu Wangu wote,” Alimaanisha kwamba watu wanapoingia katika njia sahihi na kuanza kumjua Mungu, sio pamoja tu na kila mtu kujaribiwa ndani na Shetani, bali pia waweze kujaribiwa na Shetani ndani ya kanisa lenyewe. Hata hivyo, hii ndiyo njia ambayo kila mtu anafaa kuifuata, kwa hivyo mtu yeyote asishtuke. Majaribu ya Shetani yanaweza kuja kwa aina kadhaa. Mtu anaweza kudharau au kutelekeza asemacho Mungu, na anaweza kusema mambo hasi ili kufifiza matumaini wa watu wengine, hata hivyo, yeye kwa kawaida hawashawishi watu wengine wajiunge ndani; mambo haya ni magumu kwa watu kutambua. Sababu kuu ya hili ni: Huenda bado akawa mtendaji katika kuhudhuria mikutano, lakini haelewi kuhusu maono. Kama kanisa halihadhari naye, basi kanisa lote lingeweza kushawishiwa na uhasi wake katika kumwitikia Mungu kwa uvuguvugu, hivyo kutozingatia neno la Mungu na hii ingekuwa kuanguka ndani kabisa ya majaribu ya shetani. Huenda asimuasi Mungu moja kwa moja, lakini kwa vile hawezi kuelewa neno la Mungu na hamjui Mungu, huenda akalalamika au kuwa na chuki ndani ya moyo wake. Huenda akasema kwamba Mungu amemtelekeza kwa hiyo hawezi kupata nuru na mwangaza. Huenda akataka kuondoka, lakini hisia tulivu ya woga hukaa ndani yake na huenda akasema kwamba kazi ya Mungu haitoki kwa Mungu lakini badala yake ni kazi ya pepo waovu.

Mbona Mungu humtaja Petro mara kwa mara sana? Na mbona Asema kwamba hata Ayubu hakukaribia kuwa sawa na yeye. Kusema hili hakusababishi tu kutilia maanani matendo ya Petro, bali pia inawalazimu kuweka kando mifano yote waliyonayo ndani ya mioyo yao, na hata mfano wa Ayubu—aliyekuwa na imani kuu zaidi—unapaswa kuwekwa kando pia. Ni kupitia hili tu ndio kunaweza kuwa na matokeo bora ambapo watu wanaweza kuachana na kila kitu ili kumwiga Petro, na hivyo kusonga hatua moja karibu zaidi katika kumjua Mungu. Mungu aliwaleta watu kwa njia ya utendaji ambayo Petro alifuata kumjua Mungu, ambalo lengo lake lilikuwa ni kuwapa watu jambo la rejelea. Kisha Mungu anaendelea kutabiri mojawapo ya njia ambazo Shetani atawajaribu watu Anaposema, “Lakini kama wewe huna hisia na hujali kuhusu maneno Yangu, basi bila shaka unanipinga Mimi. Hii ni kweli.” Ndani ya maneno haya, Mungu anatabiri hila za ujanja ambazo Shetani atajaribu kutumia na Anawatahadharisha watu kulizingatia kuwa onyo. Hata kama sio kila mtu atadharau neno la Mungu, hata hivyo watu wengine watatekwa na majaribu haya, kwa hiyo mwishowe Mungu asema tena kwa msisitizo, “Iwapo hamyajui maneno Yangu, hamyakubali, na wala hamyaweki katika matendo, basi bila shaka mtakuwa chombo cha kuadibu Kwangu! Nyinyi kwa hakika mtakuwa waathirika wa

Shetani!” Huu ni ushauri wa Mungu kwa wanadamu, lakini mwishowe, kama alivyotabiri Mungu, sehemu ya watu watakuwa waathiriwa wa Shetani.

Sura ya 9

Katika mawazo ya watu, Mungu ni Mungu, na mwanadamu ni mwanadamu. Mungu haneni lugha ya mwanadamu, wala mwanadamu hawezi kunena lugha ya Mungu, na kwa Mungu, madai ya mwanadamu Kwake ni rahisi, ilhali matakwa ya Mungu kwa mwanadamu hayafikiki na hayafikiriki kwa mwanadamu. Ukweli, hata hivyo, ni kinyume kabisa: Mungu anataka tu “asilimia 0.1” ya mwanadamu. Hili si la kushangaza tu kwa kila mtu, lakini pia huwafanya wahisi kukanganyikiwa sana, kama kwamba wote wamechanganyikiwa. Ni kwa msaada wa kupata nuru kwa Mungu, na neema ya Mungu tu, ndio watu hupata maarifa kidogo ya mapenzi ya Mungu. Lakini mnamo Machi 1, watu wote kwa mara nyingine walibaki wakiwa wamekanganyikiwa na wakikuna vichwa vyao. Mungu alitaka kwamba watu Wake wawe theluji inayong’aa, si mawingu yaendayo pepe. Kwa hiyo hii “theluji” inahusu nini? Na “mawingu yaendayo pepe” yanaashiria nini? Wakati huu, Mungu hasemi lolote kwa makusudi kuhusu maana ya ndani ya maneno haya. Hili linawatumbukiza watu katika kiwewe, na hivyo kuongeza imani yao wanapotafuta—kwani ni matakwa maalum kwa watu wa Mungu, na si kitu kingine, na kwa hiyo kila mtu hujikuta akitumia muda mwingi zaidi kwa hiari akifikiri kuhusu maneno haya yasiyoeleweka. Kutokana na hilo, mawazo mbalimbali huchipua ndani ya akili zao, chembe za theluji ziendazo pepe zinakuja ghafla mbele ya macho yao, na mawingu yaendayo pepe angani mara moja yanatoka katika mawazo yao. Kwa nini Mungu anataka watu Wake wawe kama theluji, na sio kama mawingu yaendayo pepe? Maana ya kweli hapa ni gani? Maneno haya hasa yanahusu nini? “Theluji” haifanyi tu mandhari yaonekane mazuri, lakini pia ni nzuri kwa ardhi ya ukulima—ni nzuri katika kuua bakteria. Baada ya kuanguka kwa theluji nyingi, bakteria zote hufunikwa na theluji inayong’aa, na uwanda wote mara moja hujaa kabisa na uhai. Vivyo hivyo, watu wa Mungu hawatakiwi tu kumjua Mungu mwenye mwili, bali pia kujinyenyekeza kwa ukweli wa kupata mwili kwa Mungu, na hivyo kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida. Hivi ndivyo theluji huyafanya mandhari kuonekana mazuri; hatimaye, ukomavu wa watu wa Mungu utalimaliza joka kuu jekundu, kuanzisha ufalme wa Mungu duniani, kueneza na kutukuza jina takatifu la Mungu, ili ufalme wote duniani ujazwe haki ya Mungu, hung’arisha miali ya Mungu, na kumemetuka na utukufu wa Mungu, na kila mahali kuna na maonyesho ya amani na ridhaa, furaha na utimizo, na uzuri unaofanya upya daima. Tauni mbalimbali zilizopo wakati wa sasa—tabia potovu ya kishetani, kama vile udhalimu, uhalifu na udanganyifu, tamaa mbovu na kadhalika—zote zinakomeshwa, na hivyo mbingu na dunia vyote vinafanywa upya. Hii ni maana ya kweli ya “baada ya kuanguka kwa theluji nyingi.” Wale ambao ni mawingu yaendayo pepe ni kama aina ya watu ambao hufuata kundi linalozungumziwa na Mungu; kama kuna majaribu ya

Shetani, au majaribio ya Mungu, wataenda pepe mara moja, na kukosa kuwepo tena. Hata kiini chao hakitasalia, kitakuwa kimetoweka kitambo sana. Kama watu ni mawingu yaendayo pepe, hawawezi tu kuishi kulingana na sura ya Mungu, lakini pia huleta aibu kwa jina la Mungu, kwani watu kama hao wako katika hatari ya kunyakuliwa wakati wowote au mahali popote, wao ni chakula ambacho Shetani hula, na wakati ambapo Shetani anawachukua kuwa mateka, watamsaliti Mungu na kumtumikia Shetani. Hili kwa dhahiri huleta aibu kwa jina la Mungu, ni kile ambacho Mungu huchukia zaidi ya yote, na ni adui za Mungu. Hivyo, wao hawana kiini cha watu wa kawaida na hawana vitendo vyenye thamani. Ni kwa sababu ya hili ndio Mungu huwa na matakwa kama haya kwa watu Wake. Lakini baada ya kuelewa kitu fulani kuhusu maneno haya, watu huwa hawajui wafanye nini baada ya hapo, kwani mada ya maneno ya Mungu imemgeukia Mungu Mwenyewe, ambalo huwaweka katika hali ngumu: “Kwa sababu Nilitoka katika nchi takatifu, si kama yungiyungi, ambalo lina jina tu na halina dutu kwa sababu lilikuja kutoka katika matope na si kutoka nchi takatifu.” Mbona, baada ya kuzungumza juu ya matakwa Yake kwa watu Wake, Mungu anaeleza kuzaliwa kwa Mungu Mwenyewe? Yawezekana kwamba kuna uwiano wa asili kati ya hayo mawili? Kweli, kuna uwiano wa asili kati ya hayo—la sivyo, Mungu hangezungumza hivyo kwa watu. Kati ya majani mabichi, yungiyungi huyumba nyuma na mbele katika upepo mwanana. Linapendeza machoni na kuthaminiwa sana. Watu hawawezi tu kutosheka nalo, na wana hamu sana ya kuogelea majini kuchuma kikonyo na kukitazama kwa karibu. Lakini Mungu asema yungiyungi linatoka matopeni, na lina jina tu wala si dutu. Inaonekana kwamba Mungu haweki umuhimu wowote kwa mayungiyungi, na kutokana na maneno Yake inaweza kuonekana kwa dhahiri kwamba Ana chuki kiasi fulani kwayo. Kotekote katika enzi, wengi wamemimina sifa kwa mayungiyungi kwa sababu hayo hutoka kwa uchafu pasipo mawaa, kiasi kwamba takriban hayawezi kulinganishwa, ni ya ajabu ya kushangaza. Machoni mwa Mungu, ingawa mayungiyungi hayana thamani—ambayo hasa ni tofauti kati ya Mungu na wanadamu. Hivyo basi inaweza kuonekana kwamba tofauti kati ya Mungu na wanadamu ni kubwa kama umbali kati ya kuba ya mbingu na msingi wa dunia. Kwa kuwa yungiyungi hutoka matopeni, virutubishi vyote linavyohitaji hutoka humo. Ni vile tu yungiyungi linaweza kujigeuza umbo, na hivyo kufurahisha macho. Watu wengi huona tu uzuri wa nje wa yungiyungi, lakini hakuna yeyote kati yao aonaye kwamba uzima ulio ndani ya yungiyungi ni mchafu na wenye najisi. Hivyo, Mungu asema kwamba lina jina tu bila dutu—ambayo ni sahihi kabisa na kweli. Na hivi hasa sivyo walivyo watu wa Mungu leo? Wao hutii na kumwamini Mungu kwa nje tu. Mbele ya Mungu, wao hujipendekeza na kujionyesha kumfanya Mungu aridhike nao; ndani, hata hivyo, wamejazwa tabia potovu ya kishetani, matumbo yao yamejaa uchafu. Hivyo, Mungu anatoa maswali kwa mwanadamu, Akiuliza kama uaminifu wake kwa Mungu umeozeshwa na uchafu, kama ni safi na kamili. Walipokuwa watendaji huduma, watu wengi walimsifu Mungu vinywani mwao lakini walimlaani mioyoni mwao. Katika vinywa

vyao, walikuwa watiifu kwa Mungu, lakini mioyoni mwao, walimuasi Mungu. Vinywa vyao vilitamka maneno hasi, na ndani ya mioyo yao walificha upinzani kwa Mungu. Kulikuweco hata na wale ambao matendo yao yalikuwa ya kulingana sawa: Waliachilia uchafu kwa vinywa vyao na kuashiria kwa mikono yao, wapotovu kabisa, wakitoa onyesho wazi na lenye kufanana na kiumbe chenye uhai la uso wa kweli wa joka kubwa jekundu. Wanastahili kweli kuitwa mayai ya joka kubwa jekundu. Lakini leo, wanasimama katika nafasi ya watendaji huduma waaminifu na kutenda kama watu waaminifu wa Mungu—aibu iliyoje! Si ajabu; walitoka matopeni, kwa hiyo hawana budi ila kuonyesha tabia yao ya halisi. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu na safi, na halisi na wa kweli, mwili Wake unatoka kwa Roho. Hili ni wazi, na bila shaka. Sio tu kuweza kushuhudia kwa Mungu Mwenyewe, bali pia kuweza kufanya kabisa mapenzi ya Mungu: huu ni upande mmoja wa dutu ya Mungu. Kwamba mwili unatoka kwa Roho na sura kuna maana kwamba mwili ambao Roho anajivisha ni tofauti kimsingi na mwili wa mwanadamu, na tofauti hii hasa iko ndani ya roho zao. Kile ambacho Roho aliye na sura kinahusu ni jinsi, kutokana na kufunika na ubinadamu wa kawaida, uungu unaweza kufanya kazi kwa kawaida ndani, ambacho si cha muujiza kabisa, na hakiwekewi mipaka na ubinadamu. “Sura ya Roho” inahusu uungu kamili, na haiwekewi mipaka na ubinadamu. Hasa, tabia ya Mungu ya asili na sura ya kweli vinaweza kuishi kwa kudhihirishwa kabisa ndani ya mwili, ambao si wa kawaida na thabiti tu, lakini wenye uadhama na ghadhabu. Mwili wa kwanza ungeweza tu kuwasilisha Mungu wa dhana za watu, yaani, Angeweza tu kutekeleza ishara na muujiza na kunena unabii. Hivyo, Hakuishi kwa kudhihirisha kabisa uhalisi wa Mungu, na kwa hiyo hakuwa mfano halisi wa Roho mwenye sura; Alikuwa tu kuonekana kwa kweli kwa uungu. Na kwa kuwa Alizidi sana uwezo wa ubinadamu wa kawaida, Hakuitwa Mungu Mwenyewe wa vitendo kamili, bali Alikuwa na kiasi kidogo cha Mungu asiye dhahiri aliye mbinguni kumhusu, alikuwa Mungu wa dhana za watu. Hii ndiyo tofauti muhimu kati ya miili miwili.

Kutoka mahali palipo juu zaidi ulimwenguni, Mungu huchunga kila mwendo wa mwanadamu, huchunga yote ambayo watu husema na kutenda. Hata kila wazo lao la ndani zaidi Hulichunguza na ubayana kabisa, bila kulipuuza—na kwa hiyo maneno ya Mungu hupenya hadi ndani ya mioyo ya watu, yakigonga kila wazo lao, na maneno Yake ni mepesi kung’amua na bila kosa. “Ingawa mwanadamu ‘anajua’ Roho Yangu, yeye pia huikosea Roho Yangu. Maneno Yangu yanaweka wazi uso mbaya wa wanadamu wote, na kuweka wazi mawazo ya ndani kabisa ya watu wote, na kusababisha wote duniani kuanguka chini katikati ya uchunguzi Wangu makini.” Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba, ingawa matakwa ya Mungu kwa mwanadamu si ya juu, watu bado hawawezi kustahimili uchunguzi makini wa Roho wa Mungu. “Ijapokuwa mwanadamu anaanguka chini, moyo wake hauthubutu kwenda mbali Nami. Miongoni mwa viumbe, ni nani asiyekuja kunipenda kwa sababu ya matendo Yangu?” Hili hata

linaashiria zaidi hekima kamili ya Mungu na kudura, na hivyo kufichua yote ambayo watu wa Mungu walifikiri walipokuwa katika cheo cha watendaji huduma: Ingawa, baada ya “biashara” iliyoishia kushindwa, “mamia ya maelfu” au “mamilioni” katika vichwa vyao ziliambulia patupu, kwa sababu ya amri za usimamizi za Mungu, na kwa sababu ya uadhama wa Mungu na ghadhabu, ingawaje waliinamisha vichwa vyao kwa huzuni, bado walimhudumia Mungu katikati ya uhasi, utendaji wao wote wa siku zilizopita ukawa maneno matupu, yaliyosahaulika kabisa; badala yake walifanya mambo kwa hiari yao ambayo yaliwafanya wao na kila mtu mwingine afurahi ili kuendelea kujiburudisha, ili kupitisha muda... Hiki ndicho kilikuwa kikiendelea kwa kweli miongoni mwa wanadamu. Hivyo, Mungu anakuwa wazi kwa mwanadamu na kusema: “Ni nani asiye kuwa na hamu kwa ajili ya kuyasikia maneno Yangu? Ni nani asiyezaliwa ndani mwake na hisia za ibada kwa sababu ya upendo Wangu?” Kusema kweli, watu wote wako radhi kukubali maneno ya Mungu, na hakuna yeyote kati yao asiyependa kusoma maneno ya Mungu—ni vile tu hawawezi kutia maneno ya Mungu katika vitendo kwa sababu wanazuiliwa na asili zao. Baada ya kusoma maneno ya Mungu, watu wengi hawawezi kustahimili kujitenga na maneno ya Mungu, na upendo kwa Mungu hufurika ndani yao. Hivyo, Mungu kwa mara nyingine Anamlaani Shetani, na mara tena Anafichua sura yake mbaya. “Enzi ambayo Shetani anaendesha ghasia na ni mdhalimu mkuu” pia ni enzi ile ile ambayo Mungu anaanza kazi Yake kuu, rasmi duniani. Kufuatia, Anaanza kazi ya kuangamiza ulimwengu. Ambalo ni kusema, kadri Shetani anavyozidi kuendesha ghasia, ndivyo siku ya Mungu inavyokaribia zaidi, na kwa hiyo ndivyo Mungu anenavyo zaidi kuhusu utukutu wa Shetani, hivyo inaonyeshwa kwamba siku ambayo Mungu ataangamiza ulimwengu inakaribia. Huu ndio utangazaji wa Mungu kwa Shetani.

Kwa nini Mungu alisema tena na tena “...na, nyuma Yangu, wao wanashiriki katika zile shughuli chafu “zenye kusifika.” Je, unafikiri kwamba mwili Ninaouvaa, haufahamu chochote kuhusu matendo yako, tabia zako, na maneno yako?” Hakusema tu maneno hayo mara moja au mbili—Kwa nini? Mara tu watu wakishafarijiwa na Mungu, na wanafahamu huzuni ya Mungu kwa ajili ya mwanadamu, ni rahisi kwao kusahau yaliyopita wanapong’ang’ana kuendelea mbele. Lakini Mungu si mwenye huruma kabisa kwa mwanadamu: Yeye huendelea kujaribu kupata fikira za watu. Hivyo Huwauliza watu mara nyingi wajijue, waache upotovu wao, kutoshiriki tena katika shughuli chafu “za kusifika,” na kutowahi kamwe kumdanganya tena Mungu aliye katika mwili. Ingawa asili za watu hazibadiliki, kuna manufaa katika kuwakumbusha mara chache. Baada ya hili, Mungu anena kutokana na mtazamo wa mwanadamu ili kufichua mafumbo yaliyo ndani yake: “Nimestahimili mvua na upepo kwa miaka mingi, na vile vile Nimepitia machungu ya ulimwengu wa binadamu, lakini ukitafakari kwa karibu, hakuna kiasi cha mateso kinachoweza kumfanya mwanadamu aliye katika nyama za mwili kupoteza matumaini ndani Yangu, kama vile hakuna utamu wowote unaoweza kumfanya

mwanadamu wa mwili awe bila hisia, mwenye kuvunjika moyo au mwenye kunipuuza Mimi Je, upendo wa mwanadamu Kwangu ni mdogo kiasi kwamba upo tu katikati ya ama kutokuwa na maumivu au kutokuwa na utamu?” “Yote chini ya jua ni tupu,” maneno haya kweli yana maana ya ndani. Hivyo Mungu asema kwamba hakuna chochote kinachoweza kumfanya mwanadamu akate tamaa Kwake au kumdharau. Ikiwa watu hawampendi Mungu, ni heri basi wafe; ikiwa hawampendi Mungu, basi mateso yao ni bure, na furaha wanayoifurahia ni tupu, na imeongezewa kwa dhambi zao. Kwa vile hakuna hata mtu mmoja anayempenda Mungu kweli, hivyo Asema, “Je, upendo wa mwanadamu Kwangu ni mdogo kiasi kwamba upo tu katikati ya ama kutokuwa na maumivu au kutokuwa na utamu?” Katika ulimwengu wa mwanadamu, mtu yeyote angewezaje kuishi bila maumivu au utamu? Mara kwa mara, Mungu asema, “Hakuna hata mtu mmoja amewahi kuuona uso Wangu kweli na amewahi kusikia sauti Yangu kweli, kwani mwanadamu hanijui kweli.” Mungu asema kwamba mwanadamu hamjui Yeye kweli, lakini kwa nini Anataka mwanadamu amjue? Je, huu si ukinzani? Kila mojawapo ya maneno ya Mungu lina lengo fulani. Kwa kuwa wanadamu wamekuwa wenye ganzi, Mungu anatumia kanuni ya kufanya 100% ya kazi Yake ndani ya mwanadamu ili hatimaye kutimiza asilimia 0.1 ndani ya moyo wa mwanadamu. Hiyo ndiyo mbinu ambayo Mungu hufanyia kazi, na Mungu lazima atende hivyo ili kutimiza malengo Yake. Hii pia ni hekima ya maneno ya Mungu kabisa. Je, mmelewa hili?

Mungu asema: “Ninapozionyesha siri Zangu wazi na kufanya wazi mapenzi Yangu katika mwili, hamwoni haya yote; mnaisikiliza sauti, lakini hamwelewi maana yake. Mimi hukumbwa na huzuni kuu. Ingawa Mimi Niko katika mwili, Ninakosa uwezo wa kufanya kazi ya huduma ya mwili.” Katika suala moja, maneno haya huwafanya watu, kwa ajili ya ganzi yao, kuanza kushirikiana na Mungu; katika suala lingine, Mungu hufichua sura ya kweli ya uungu Wake katika mwili. Kwa kuwa kimo cha watu ni kidogo sana, ufunuo wa uungu wakati wa kipindi ambacho Mungu yuko ndani ya mwili ni kufuatana tu na uwezo wa mwanadamu wa kukubali. Wakati wa hatua hii ya kazi, watu wengi hubaki wasioweza kuwa na ridhaa kamili, ambalo linaonyesha kwa kiasi cha kutosha vile uwezo wao wa ridhaa ni hafifu. Hivyo, uungu hautekelezi kwa ukamilifu kazi yake ya asili unapofanya kazi; hii ni sehemu ndogo tu. Hili linaonyesha kwamba katika kazi ya siku za baadaye, uungu utafichuliwa polepole kufuatana na hali ya kupatikana tena kwa mwanadamu. Uungu, hata hivyo, haukui polepole, lakini ni kile ambacho Mungu mwenye mwili anacho kimsingi, na si kama kimo cha mwanadamu.

Kulikuwa na lengo na maana kwa Mungu kumuumba mwanadamu, na hivyo Mungu asema, “Kama mwanadamu angeangamizwa na ghadhabu Yangu, umuhimu wa kuumba Kwangu kwa mbingu na dunia ungekuwa nini?” Baada ya mwanadamu kupotoshwa, Mungu alipanga upataji wa sehemu ya watu kwa sababu ya kujifurahisha Kwake; si kweli kwamba watu wote

wanatakiwa kuangamizwa, au kwamba watang’olewa wakikiuka hata kidogo amri za usimamizi za Mungu. Haya si mapenzi ya Mungu. Kama alivyosema Mungu, hilo halingekuwa na maana. Ni hasa kwa sababu ya “kutokuwa na maana” huku ndiyo hekima ya Mungu inafanywa kuwa wazi. Je, hakuna umuhimu mkuu zaidi kwa Mungu kuzungumza na kutenda kazi kwa njia nyingi ili kuadibu, kuhukumu, na kuwagonga watu wote, hatimaye kuchagua wale wanaompenda kweli? Na ni kwa njia hii hasa ndio matendo ya Mungu hufichuliwa, kwa hiyo uumbaji wa mwanadamu unakuwa wa maana zaidi. Hivyo, mengi ya maneno ya Mungu huelea yakienda; hili ni ili kutimiza lengo, na huu pekee ndio uhalisi wa baadhi ya maneno Yake.

Nyongeza: Sura ya 1

Ninachotaka mfanye si nadharia isiyo dhahiri na tupu ambayo Naizungumzia, wala si kitu cha kutofikirika na akili ya mwanadamu au kisichoweza kutimizwa na mwili wa mwanadamu. Ni nani anayeweza kuwa mwaminifu kabisa ndani ya nyumba Yangu? Na ni nani anayeweza kutoa nafsi yake yote ndani ya ufalme Wangu? Kama si ufunuo wa mapenzi Yangu, je, mngeweza kujitilia matakwa ambayo mnaridhisha moyo Wangu? Hakuna yeyote ambaye amewahi kuufahamu moyo Wangu, na hakuna yeyote ambaye amewahi kutambua mapenzi Yangu. Ni nani amewahi kuuona uso Wangu au kuisikia sauti Yangu? Petro alifanya hivyo? Au Paulo? Au Yohana? Au Yakobo? Ni nani amewahi kuvishwa na Mimi, au kumilikiwa na Mimi, au kutumiwa na Mimi? Ijapokuwa mara ya kwanza Nilipoupata mwili ilitendeka ndani ya uungu, mwili ambao Nilijivika haukujua mateso ya mwanadamu, kwa sababu Sikuwa mwili katika mfano, kwa hiyo haingeweza kusemwa kwamba mwili ulifanya mapenzi Yangu kikamilifu. Ni wakati tu ambapo uungu Wangu unaweza kufanya jinsi Ningetenda na kunena jinsi Ningenena katika nafsi ya ubinadamu wa kawaida, bila kipingamizi au kizuizi, ndipo inaweza kusemwa kwamba mapenzi Yangu yamefanyika katika mwili. Kwa vile ubinadamu Wangu wa kawaida unaweza kuukinga uungu Wangu, hivyo lengo Langu la kuwa mnyenyekevu na Aliyefichika linatimizwa. Wakati wa hatua ya kazi katika mwili, ingawa uungu unatenda moja kwa moja, si rahisi kwa watu kuona vitendo kama hivyo, ambalo ni kwa sababu tu ya maisha na vitendo vya ubinadamu wa kawaida. Kupata mwili huku hakuwezi kufunga kwa siku 40 kama kupata mwili kwa mara ya kwanza, lakini Anafanya kazi na kunena kwa kawaida, na ingawa Anafichua siri, Yeye ni wa kawaida kabisa; Yeye ni wa kawaida kabisa; sivyo jinsi watu wanavyodhani—sauti Yake sio kama radi, uso Wake haumemetuki kwa nuru, na mbingu hazitetemeki Anapotembea. Ingelikuwa hivyo, basi hakungekuwa na hekima Yangu yoyote katika jambo hili, na haingewezekana kumwaibisha na kumshinda Shetani.

Wakati ambapo Ninaonyesha uungu Wangu chini ya ulinzi wa ubinadamu wa kawaida, Ninatukuzwa kabisa, kazi Yangu kuu inatimizwa, na hakuna chochote kinachosababisha

matatizo yoyote. Hii ni kwa sababu lengo la kupata mwili Kwangu hasa ni kuwaruhusu wale wote wanaoniamini wayaone matendo ya uungu Wangu katika mwili, na kumwona Mungu Mwenyewe wa vitendo, hivyo kuondoa katika mioyo ya watu nafasi ya Mungu asiyeonekana na Asiyeshikika. Kwa kuwa Nala, Najivisha nguo, Nalala, Naishi, na kutenda kama mtu wa kawaida, kwa kuwa Nazungumza na kucheka kama mtu wa kawaida, nami Nina mahitaji ya mtu wa kawaida, na pia Nina dutu ya uungu kamili, Ninaitwa “Mungu wa vitendo.” Jambo hili si dhahania, nalo ni rahisi kuelewa; linaweza kuonekana katika sehemu ambayo kiini cha Kazi Yangu kimo, na katika awamu ya kazi ambamo lengo Langu liko. Kufichua uungu Wangu kupitia kwa ubinadamu wa kawaida ni lengo kuu la kupata mwili Kwangu. Si vigumu kuona kwamba kiini cha kazi Yangu kiko katika sehemu ya pili ya enzi ya hukumu.

Ndani Yangu, hakujawahi kuwa na maisha ya binadamu au dalili ya binadamu. Maisha ya binadamu hayajawahi kushikilia nafasi ndani Yangu, na hayajawahi kukomesha ufichuzi wa uungu Wangu. Hivyo, kadri Mtu anavyoionyesha sauti Yangu mbinguni na mapenzi ya Roho Wangu, ndivyo Anavyoweza kumwaibisha Shetani zaidi, na ndivyo inavyokuwa rahisi zaidi kufanya mapenzi Yangu katika ubinadamu wa kawaida. Hili pekee limemshinda Shetani, na tayari Shetani ameaibishwa kabisa. Ingawa Nimefichika, hili halizuii matamshi na vitendo vya uungu Wangu—ambalo linatosha kuonyesha kwamba Nimekuwa mshindi, na Nimetukuzwa kabisa. Kwa kuwa kazi Yangu katika mwili haina kipingamizi, na kwa kuwa Mungu wa vitendo sasa Ana nafasi ndani ya mioyo ya watu na Amekita mizizi ndani ya mioyo yao, inathibitishwa kabisa kwamba Shetani ameshindwa na Mimi. Na kwa kuwa Shetani hawezi kufanya lolote zaidi miongoni mwa wanadamu, na ni vigumu kuifunda sifa ya Shetani katika mwili wa mwanadamu, mapenzi Yangu yanaendelea bila kipingamizi. Maudhui ya kazi Yangu, hasa, ni kuwasababisha watu wote wayatazame matendo Yangu ya ajabu na kuuona uso Wangu halisi: Mimi si asiyeweza kufikika, Siendi juu sana katika anga, Mimi si asiye na umbo wala sura maalum. Mimi si asiyeonekana kama hewa, wala si kama wingu linaloelea, linaloweza kupeperushwa kwa urahisi; badala yake, ingawa Naishi miongoni mwa wanadamu, na kupitia utamu, uchachu, uchungu, na ukali miongoni mwa wanadamu, mwili Wangu unatofautiana kimsingi na ule wa mwanadamu. Watu wengi hushindwa kushirikiana na Mimi, lakini wengi pia hutamani kushirikiana na Mimi. Ni kana kwamba kuna siri kubwa, zisizoeleweka ndani ya Mungu aliyepata mwili. Kwa sababu ya ufunuo wa wazi wa uungu, na kwa sababu ya ulinzi wa kuonekana kwa mwanadamu, watu hukaa mbali sana nami, wakiamini kwamba Mimi ni Mungu mwenye huruma na upendo, lakini pia wanauogopa uadhama na ghadhabu Yangu. Hivyo, ndani ya mioyo yao, wanataka kuzungumza nami kwa dhati, lakini hawawezi kufanya watakavyo—kile ambacho mioyo yao inatamani, wanakosa nguvu. Hivyo ndivyo zilivyo hali za kila mtu katika hali hii—na kadri watu walivyo namna hii, ndivyo thibitisho la ufunuo wa hali mbalimbali

za tabia Yangu lilivyo kuu zaidi, hivyo kutimiza lengo la watu kujua kuhusu Mungu. Lakini hili ni la baadaye; kilicho muhimu ni kuwafanya watu wayajue matendo Yangu ya ajabu kutokana na shughuli za mwili Wangu, zikiwasababisha kujua dutu ya Mungu: Kama wanavyodhani watu, Mimi si asiye wa kawaida na wa mwujiza; badala yake, Mimi ni Mungu wa vitendo aliye wa kawaida katika mambo yote. Nafasi “Yangu” katika dhana za watu imeondolewa, na wao huja kunijua kwa kweli. Ni wakati huo tu ndipo Mimi huchukua nafasi Yangu ya kweli katika akili zao.

Mbele ya watu wote, Sijawahi kufanya tu kitu chochote cha ajabu ambacho kimethaminiwa na watu, bali pia Mimi ni wa kawaida mno; Siwaruhusu watu kuona chochote kilicho na dalili ya Mungu katika mwili Wangu kwa makusudi. Lakini kwa sababu ya maneno Yangu, watu wanashindwa kabisa, na wanautii ushuhuda Wangu. Ni hivyo tu ndivyo watu huja kujua, bila wasiwasi, Mimi niliye katika mwili juu ya msingi wa kuamini kabisa kwamba Mungu yupo kweli. Kwa njia hii, ufahamu wa watu kunihusu huwa halisi zaidi, dhahiri zaidi, na hautiwi doa hata kidogo kwa mwenendo wao mzuri; yote ni matokeo ya uungu Wangu kutenda moja kwa moja, ukiwapa watu ufahamu mkuu zaidi wa uungu Wangu, kwani uungu pekee ndiyo sura halisi ya Mungu na sifa ya asili ya Mungu—watu wanapaswa kuona hili. Nitakacho ni maneno, vitendo, na matendo yaliyo katika uungu—Sijali kuhusu maneno na vitendo katika ubinadamu. Lengo Langu ni kuishi na kutenda katika uungu—Sitaki kukita mizizi na kuchipua katika ubinadamu, Sitaki kuishi katika ubinadamu. Je, mnaelewa Ninachosema? Ijapokuwa Mimi ni mgeni katika ubinadamu, Sitaki hili; Natenda katika uungu kamili, na ni kwa njia hii tu ndiyo watu wanaweza kuufahamu uso Wangu halisi vizuri zaidi.

Sura ya 10

Katika wakati wa ujenzi wa kanisa, Mungu alitaja ujenzi wa kanisa kwa nadra. Hata Alipotaja, Alifanya hivyo katika lugha ya wakati wa ujenzi wa kanisa. Mara tu Enzi ya Ufalme ilipokuja, Mungu alifuta mbinu na wasiwasi nyingine za wakati wa ujenzi wa kanisa mara mmoja na Hakuwahi tena kusema hata neno moja kuuhusu. Hii hasa ni maana ya msingi ya “Mungu Mwenyewe” ambaye daima ni mpya na kamwe si mzee. Hata kama vitu vilifanywa vizuri katika siku za zamani, kwa kadri vilivyo sehemu ya enzi iliyopita, Mungu anaviweka vitu kama hivyo katika kundi la vitu vinavyotokea katika wakati kabla ya Kristo, huku wakati wa sasa ukijulikana kama wakati wa “baada ya Kristo^[a].” Kuhusu suala hili, ujenzi wa kanisa unaweza kuchukuliwa kama kitangulizi cha lazima cha ujenzi wa ufalme. Uliweka msingi kwa Mungu kutumia nguvu Zake kuu katika ufalme. Leo, kazi ya ujenzi wa kanisa ni kinda la ndege la ujenzi wa ufalme tu, ambalo ni lengo la msingi la kazi ya Mungu duniani. Mungu alitayarisha utondoti wote wa kazi Yake kabla ya kumalizika kwa kazi ya ujenzi wa kanisa, na wakati ulipokuwa sawa, Alianza kazi

Yake moja kwa moja. Hasa, Mungu alinena hivi, “Enzi ya Ufalme ni, hata hivyo, tofauti na nyakati za kale. Haihusu jinsi ambavyo binadamu hutenda; badala yake, Nimeshuka duniani ili Nitekeleze kazi Yangu binafsi, jambo ambalo wanadamu hawawezi kuelewa wala kufanikisha.” Kwa kweli, kazi hii lazima itekelezwe na Mungu binafsi—hakuna mwanadamu anayeweza kazi kama hii, yeye hana uwezo unaohitajika. Mbali na Mungu, ni nani angetekeleza kazi kubwa kama hii miongoni mwa wanadamu? Ni nani mwingine anaweza “kuwatesa” wanadamu wote hadi kukaribia kufa? Je, wanadamu wangeweza kuipanga kazi kama hii iwezekanavyo? Ni kwa nini Anasema, “Mimi binafsi Natekeleza kazi Yangu baada ya kushuka duniani”? Je, Roho wa Mungu angeweza kutoweka kweli kutoka kwa anga yote? “Mimi binafsi Natekeleza kazi Yangu baada ya kushuka duniani,” inahusu ukweli kwamba Roho wa Mungu anakuwa mwili ili kutenda kazi, na ukweli kwamba Roho wa Mungu anafanya kazi kwa dhahiri kupitia kwa wanadamu. Kwa kutekeleza kazi Yake binafsi, Mungu anawaruhusu watu wengi kumwona Mungu Mwenyewe kwa macho yao, ili wasihitaji kutafuta kwa makini ndani ya roho zao. Zaidi ya hayo, linawaruhusu wanadamu wote kuona matendo ya Roho kwa macho yao wenyewe na kuwaonyesha kwamba kuna tofauti muhimu kati ya mwili wa mwanadamu na ule wa Mungu. Sawia, kotekote katika anga yote na ulimwengu dunia wote, Roho wa Mungu bado Anafanya kazi. Wale watu wote ambao wamepata nuru, kwa vile wamekubali jina la Mungu, wanaona jinsi Roho wa Mungu hufanya kazi na, hivyo, hufahamiana hata zaidi na kupata mwili kwa Mungu. Hivyo, kama tu uungu wa Mungu utafanya kazi moja kwa moja, yaani Roho wa Mungu aweze kufanya kazi bila kizuizi hata kidogo, ndio mwanadamu anaweza kufahamiana zaidi na Mungu Mwenyewe wa vitendo. Hiki ni kiini cha ujenzi wa ufalme.

Mungu amekuwa mwili mara ngapi? Yaweza kuwa mara kadhaa? Ni kwa nini Mungu amesema mara nyingi, “Wakati mmoja Nilishuka kwenye ulimwengu wa binadamu Nikapitia na Nikaangalia kwa makini mateso yao lakini nilifanya hivyo bila ya kutimiza lengo la kupata mwili Kwangu”? Je, ni kweli kwamba Mungu amekuwa mwili mara kadhaa, lakini hajawahi kamwe kujulikana na mwanadamu hata mara moja? Kauli hii haimaanishi hivi. Mara ya kwanza Mungu alipokuwa mwili, lengo Lake kwa kweli halikuwa mwanadamu amjue. Badala yake, Alitekeleza kazi Yake na kisha akaondoka bila mtu yeyote kutambua au hata kuwa na nafasi ya kumjua. Hakumruhusu mwanadamu kumjua kwa ukamilifu na pia hakumiliki kabisa umuhimu wa kupata mwili, kwa hiyo Hangeweza kusemekana kuwa mwili kwa ukamilifu. Katika kupata mwili kwa mara ya kwanza, Alitumia tu umbo la mwili ambao haukuwa na asili ya dhambi kutekeleza kazi hiyo—kazi ilipokuwa imekamili, hakukuwa na haja ya kutaja zaidi. Kuhusu wale watu ambao wametumiwa na Mungu kotekote katika enzi, mifano kama hiyo haistahili hata kidogo kuitwa kupata mwili. Leo, Yule ambaye ni Mungu Mwenyewe wa vitendo pekee, Aliye na sura ya nje ya ubinadamu wa kawaida inayoficha uungu kamili ndani, na ambaye lengo Lake

ni kumruhusu mwanadamu kumjua ndiye Anaweza kuitwa kwa ukamilifu kupata mwili. Maana ya ziara ya Mungu ya kwanza kwa ulimwengu huu ina hali moja tu yenye umuhimu wa kile kinachoitwa leo kupata mwili—ziara hii katu haikuwa na maana kamili ya kile kinachoitwa sasa kupata mwili. Hii ndiyo sababu Mungu alisema, “bila kutimiza umuhimu wa kupata mwili.” “Kupitia na kuchunguza mateso ya mwanadamu” kunahusu Roho wa Mungu na aina mbili za kupata mwili, hivyo Mungu alisema, “Punde ujenzi wa ufalme ulipoanza, Mimi nikiwa mwili nilianza rasmi kutekeleza huduma Yangu; yaani, Mfalme wa ufalme rasmi Alichukua ukuu wa mamlaka Yake makuu.” Ingawa ujenzi wa kanisa ulikuwa ushuhuda kwa jina la Mungu, kazi haikuwa imeanza rasmi—ni leo tu ndiyo inaweza kusemekana kuwa ujenzi wa ufalme. Yote yaliyofanywa awali yalikuwa limbuko tu, halikuwa jambo halisi. Ingawa ilisemekana kwamba ufalme ulikuwa umeingiwa, bado hakukuwa na kazi iliyokuwa ikifanywa ndani yake. Leo tu, vile sasa kazi inafanywa ndani ya uungu wa Mungu na Mungu ameanza rasmi kazi Yake ndipo mwanadamu hatimaye ameingia katika ufalme. Hivyo, “mshuko wa ufalme katika ulimwengu wa binadamu—mbali na kuwa tu suala la maonyesho ya moja kwa moja—ni wa ukweli halisi; hiki ni kipengele mojawapo cha maana ya ‘uhalisi wa kutenda.’” Dondoo hili ni muhtasari wa kufaa wa ufafanuzi wa hapo awali. Baada ya kutoa ufafanuzi huu, Mungu anaendelea mbele kueleza sifa za hali ya jumla ya wanadamu, Akimwacha mwanadamu katika hali ya kujishughulisha kwa siku zote. “Kotekote katika ulimwengu, binadamu wote hukaa chini ya upendo Wangu, huruma Yangu, lakini pia binadamu wote hukaa chini ya hukumu Yangu, na vivyo hivyo chini ya majaribio Yangu.” Maisha ya mwanadamu huongozwa kufuatana na kanuni na sheria fulani, ambazo Mungu ameweka. Kanuni na sheria hizi ni zifuatazo: Kutakuwa na nyakati za furaha, nyakati za kuvunjika moyo na zaidi, nyakati za usafishaji wa dhiki za kustahimili. Hivyo, hakuna mwanadamu atakayeishi maisha ya furaha tupu au mateso tupu. Kila maisha yatakuwa na milima na mabonde yake. Kwa wanadamu wote, sio tu kwamba upendo na huruma wa Mungu pekee ni dhahiri, ila pia hukumu Yake na tabia Yake kamili. Inaweza kusemekana hivi: Inaweza kusemekana hivi: Wanadamu wote huishi kupitia kwa majaribio ya Mungu, sivyo? Kote ulimwengu huu mkubwa, wanadamu wote hufanya kazi kwa kujishughulisha katika kazi ya kutafuta njia yao wenyewe. Hawana hakika wajibu wao ni gani na wengine hata huharibu au hupoteza maisha yao kwa ajili ya majaliwa yao. Hata Ayubu hakuwa tofauti na wengine: Akishinda majaribio mengi ya Mungu, yeye hata hivyo aliendelea kutafuta njia yake mwenyewe. Hakuna mwanadamu anayeweza kubaki palepale kupitia kwa majaribio ya Mungu. Kwa sababu ya ulafi wake au asili yake ya binadamu, hakuna mwanadamu anayeridhishwa kabisa na hali yake ya sasa, na hakuna mwanadamu anayeweza kubaki palepale kupitia kwa majaribio: Kila mwanadamu huvunjika chini ya hukumu ya Mungu. Kama Mungu angeendelea kuwa makini sana na mwanadamu, kama Angeendelea kushikilia madai ya kushurutisha kama hayo kwa mwanadamu, ingekuwa tu kama alivyosema Mungu: “jamii nzima

ya binadamu ingeporomoka chini ya macho Yangu ya kuchoma.”

Licha ya ukweli kwamba ujenzi wa ufalme umeanza rasmi, maamkuzi kwa ufalme bado hayajatangazwa rasmi—sasa ni unabii tu wa kile kitakachokuja. Wakati ambapo watu wote watakuwa wamefanywa kamili na mataifa yote ya dunia kugeuka kuwa ufalme wa Kristo, basi huo utakuwa wakati ambapo radi saba zitanguruma. Siku ya sasa ni hatua ndefu ya kwenda mbele katika mwelekeo wa hatua hiyo, shambulio limeachiliwa huru kwa muda ujao. Huu ni mpango wa Mungu—hivi karibuni utafanikishwa. Hata hivyo, Mungu tayari amefanikisha yote ambayo Amesema. Hivyo, ni dhahiri kwamba mataifa ya dunia ni makasri tu yaliyo mchangani yanayotetemeka bamvua linapokaribia: Siku ya mwisho iko karibu sana na joka kubwa jekundu litaanguka chini ya neno la Mungu. Ili kuhakikisha kwamba mpango wa Mungu unatekelezwa kwa ufanisi, malaika wa mbinguni wameshuka juu ya dunia, wakifanya kila wanaloweza kumridhisha Mungu. Mungu Mwenyewe mwenye mwili Amejipanga katika uwanja wa vita kupigana na adui. Po pote ambapo Aliyepata mwili huonekana, adui anaangamiziwa mahali hapo. Uchina ni ya kwanza kuangamizwa, kuharibiwa kabisa kwa mkono wa Mungu. Mungu haipi Uchina upande wowote kabisa. Thibitisho la kuendelea kuanguka kwa joka kubwa jekundu linaweza kuonekana katika ukomavu wa watu unaoendelea. Hili linaweza kuonekana wazi na mtu yeyote. Ukomavu wa watu ni ishara ya kifo cha adui. Huu ni ufafanuzi kidogo wa kile kinachomaanishwa na “kufanya vita.” Hivyo, Mungu aliwakumbusha watu wakati mwingi watoe ushuhuda mzuri kwa Mungu kutangua hali ya fikira, ubaya wa joka kubwa jekundu ndani ya mioyo ya wanadamu. Mungu hutumia kumbusho kama hizo kuchangamsha imani ya mwanadamu na, kwa kufanya hivyo, Hutimiza ujuzi katika kazi Yake. Hili ni kwa sababu Mungu amesema, “Binadamu ana uwezo wa kufanya nini? Si ni afadhali Nifanye hivyo Mwenyewe?” Wanadamu wote wako hivyo. Si kwamba wao hawawezi tu, bali pia huvunjika moyo na husikitishwa kwa urahisi. Kwa sababu hii, hawawezi kumjua Mungu. Mungu hafufui tu imani ya mwanadamu, kwa siri Yeye humjaza mwanadamu nguvu siku zote.

Linalofuata, Mungu alianza kunena kwa ulimwengu wote. Mungu hakuanzisha tu kazi Yake mpya Uchina, Kotekote ulimwenguni Alianza kufanya kazi mpya ya leo. Katika hatua hii ya kazi, kwa vile Mungu anataka kufichua matendo Yake yote kotekote katika dunia ili wanadamu wote ambao wamemsaliti watakuja tena kuinama kwa utiifu mbele ya kiti Chake cha enzi, hivi ndani ya hukumu ya Mungu bado kuna huruma na upendo wa Mungu. Mungu hutumia matukio ya sasa kotekote ulimwenguni kutetemesha mioyo ya wanadamu, Akiamsha kumtafuta Mungu ili waweze kumiminika kwenda Kwake. Hivyo Mungu asema, “Hii ni mojawapo ya njia ambazo Nafanya kazi, na bila shaka ni kitendo cha ukombozi kwa ajili ya mwanadamu, na kile Ninachompa bado ni aina ya upendo.” Mungu anafichua asili halisi ya mwanadamu kwa usahihi upenyao, usio na kifani, na usiohitaji bidii. Hili humwacha mwanadamu akiuficha uso wake kwa

aibu, akiwa amefedheheshwa kabisa. Kila wakati Mungu anenapo, kwa kiasi fulani Yeye daima hutaja hali fulani ya unyonge wa mwanadamu ili, kwa raha zake, mwanadamu asisahau kujijua na asifikirie kujijua ni kazi ya kale. Njiaavyo asili ya mwanadamu, kama Mungu angekosha kutaja makosa yake kwa dakika moja tu, mwanadamu angegeuka kuwa mpotovu na mwenye kiburi. Hivyo, leo Mungu asema, “Binadamu—mbali na kuthamini vyeo ambavyo Nimeweka juu yao, wengi wao, kwa sababu ya jina ‘watendaji-huduma,’ wanaweka chuki katika nyoyo zao, na wengi sana, kwa sababu ya jina ‘watu Wangu,’ huzalisha upendo Kwangu katika nyoyo zao. Hakuna anayepaswa kujaribu kunidanganya; macho Yangu huona kila kitu!” Punde tu mwanadamu aonapo kauli hii, yeye huwa na wasiwasi mara moja. Yeye huhisi kwamba matendo yake ya zamani hayakuwa yamepevuka—aina ya udanganyifu tu unaomkosea Mungu. Ametaka kumridhisha Mungu hivi karibuni, lakini huku akiwa radhi kupita kiasi, anakosa nguvu na hajui analopaswa kufanya. Bila kukusudia, anatiwa moyo na azimio lililotiwa nguvu. Hili ndilo tokeo la kusoma maneno haya mtu anapokuwa ametulia.

Kwa upande mmoja, Mungu asema kwamba Shetani ni mwenye wazimu mno, huku kwa upande mwingine Asema pia wanadamu wengi sana hawabadilishi asili yao ya kale. Kutokana na hili, ni dhahiri kwamba matendo ya Shetani hudhihirishwa kupitia kwa mwanadamu. Hivyo, Mungu humkumbusha mwanadamu mara kwa mara asiwe mpotovu, asije akamezwa na Shetani. Huku si kutoa unabii tu kwamba watu wengine wataasi, zaidi ni kengele inayolia kuonya watu wote waachane na yaliyopita haraka na watafute yale ambayo ni ya wakati wa sasa. Hakuna mwanadamu anayetamani kupagawa na mashetani au kujawa na pepo waovu, kwa hiyo neno la Mungu hata zaidi ni onyo na kuasa kwao. Hata hivyo, watu wengi wanapoenda kinyume kupita kiasi, wakitilia maanani sana kila neno la Mungu, Mungu kwa zamu husema, “Wengi wa watu wanasubiri Nifichue mafumbo zaidi ili walishe macho yao. Ihali, iwapo utakuja kuelewa siri zote za mbinguni, je, ni nini utakalofanya na hayo maarifa? Je, yataweza kuongeza upendo wako Kwangu? Je, yatachochea upendo wako Kwangu?” Kutokana na hili ni dhahiri kwamba mwanadamu hatumii neno la Mungu kumjua Mungu na kumpenda Mungu, lakini badala yake kuongeza maduka ya “kijighala chake.” Kwa hiyo, Mungu kutumia msemu “walishe macho yao” kueleza kutokuwa kadiri kwa mwanadamu kunadhihirisha jinsi upendo wa mwanadamu kwa Mungu bado si safi kwa ukamilifu. Kama Mungu hangetandua siri hizo, mwanadamu hangetilia maanani sana maneno Yake, lakini badala yake angeyaangalia kidogo tu, kuyatazama mara moja, kana kwamba anapendezwa na maua akienda shoti mgongoni mwa farasi. Hangechukua wakati kutafakari na kuyafikiria kweli maneno Yake. Watu wengi sana hawahifadhi kwa upendo mkubwa neno la Mungu. Hawafanyi kila linalowezekana kula na kunywa maneno Yake, lakini badala yake huyapitia juujuu upesi kwa uzembe. Kwa nini Mungu ananena sasa kwa njia tofauti kulika nyakati zilizopita? Kwa nini yote ni lugha isiyofahamika? Kwa mfano, “kuwavisha”

katika “Mimi kamwe Singewahi kamwe kuwavisha watu taji na vitambulisho hivi kwa kawaida,” “dhahabu safi zaidi” katika “Yupo ambaye anaweza kupokea ndani ya nafsi yake dhahabu safi zaidi ambayo maneno Yangu yanaundwa nayo,” Kutaja kwake awali “usindikaji” katika “bila kupitia usindikaji wowote na Shetani” na misemo mingine kama hiyo. Mwanadamu haelewi ni kwa nini Mungu hunena kwa njia hii. Hafahamu ni kwa nini Yeye hunena kwa njia kama hii ya mzaha, ya ucheshi na ya kuchokoza. Hili hasa ni dhihirisho la kusudi la kunena kwa Mungu. Tangu mwanzo kabisa mpaka sasa, mwanadamu daima hajaweza kufahamu neno la Mungu na imeonekana kana kwamba neno la Mungu kweli lilikuwa la mashaka sana na kali. Kwa kuongeza mkazo mdogo sana wa ucheshi—kuongeza mzaha hapa na pale—Anaweza kufanya hali kuwa angavu na maneno Yake na kumruhusu mwanadamu kutuliza misuli yake kidogo. Kwa kufanya hivyo, Anaweza kutimiza hata matokeo makubwa zaidi, Akiwashurutisha wanadamu wote kutafakari juu ya neno la Mungu.

Tanbihi:

a. “Baada ya Kristo” ina maana ya “AD (Anno Domini).”

Sura ya 11

Kwa macho ya mwanadamu, inaonekana hakuna badiliko katika matamshi ya Mungu wakati wa kipindi hiki, ambalo ni kwa sababu watu hawawezi kuelewa sheria ambazo kwazo Mungu hunena, na hawafahamu muktadha wa maneno Yake. Baada ya kusoma maneno ya Mungu, watu hawaamini kwamba kuna mafumbo yoyote mapya katika maneno haya; hivyo, hawawezi kuishi maisha yaliyo mapya kiajabu, na badala yake huishi maisha yaliyokwama na yasiyokuwa na uhai. Lakini katika matamshi ya Mungu, tunaona kwamba kuna kiwango cha kina cha maana, kile kisichofahamika na pia kisichofikika na mwanadamu. Leo, kwa mwanadamu kubahatika vya kutosha kusoma maneno kama hayo ya Mungu ni baraka kuu zaidi ya zote. Kama hakuna ambaye angesoma maneno haya, mwanadamu daima angesalia mwenye kiburi, wa kujidai, asiyejijua, na asiye fahamu tu ni dosari ngapi alizo nazo. Baada ya kusoma maneno ya Mungu yenye maana sana, yasiyoeleweka, watu huyastaajabia kisiri, na kuna kusadikisha kwa kweli ndani ya mioyo yao, isiovunda na uwongo; mioyo yao huwa mfano halisi, siyo bidhaa za kughushi. Hili ndilo hufanyika kwa kweli ndani ya mioyo ya watu. Kila mtu ana hadithi yake mwenyewe moyoni mwake. Ni kana kwamba wanajiambia wenyewe: Huenda hili lilinenwa na Mungu Mwenyewe—kama si Mungu, nani mwingine angetamka maneno kama haya? Mbona siwezi kuyanena? Mbona mimi siwezi kufanya kazi kama hiyo? Inaonekana Mungu aliyepata mwili ambaye Mungu huzungumzia kweli ni halisi, naye ni Mungu Mwenyewe! Sitakuwa na shaka tena. La sivyo, huenda hata ikawa kwamba wakati ambapo mkono wa Mungu utafika, muda wa majuto utakuwa umepita mno! ... Hiki ndicho watu wengi

sana hufikiria ndani ya mioyo yao. Ni haki kusema kwamba, tangu wakati ambapo Mungu alianza kunena mpaka leo, watu wote wangukuwa wamepotea bila msaada wa maneno ya Mungu. Mbona husemekana kwamba kazi hii yote hufanywa na Mungu Mwenyewe, na sio na mwanadamu? Mungu asingetumia maneno kuyasaidia maisha ya kanisa, kila mtu angetoweka bila dalili. Je, hii si nguvu ya Mungu? Hii kweli ni lugha ya kushawishi ya mwanadamu? Je, hii ni vipaji vya ajabu vya mwanadamu? Bila shaka la! Bila uchunguzi, hakuna ambaye angejua ni aina gani ya damu hutiririka katika vena zake, hawangefahamu ni mioyo mingapi waliyo nayo, au bongo ngapi, na wote wangefikiri kwamba wanamjua Mungu. Hawajui kwamba bado upinzani upo ndani ya ufahamu wao? Si ajabu kwamba Mungu husema, “Kila mtu katika wanadamu anapaswa kukubali uchunguzi wa Roho Wangu, anapaswa kuchunguza kwa makini kila neno na kitendo chake, na, zaidi ya hayo, anapaswa kuangalia matendo Yangu ya ajabu.” Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba maneno ya Mungu si yasiyo na lengo maalum na kutokuwa na msingi. Mungu hajawahi kamwe kumtendea mtu yeyote bila haki; hata Ayubu, na imani yake yote, hakusamehewa—yeye pia alichunguzwa, na kuachwa bila mahali popote pa kujificha kutokana na aibu yake. Na sembuse watu wa leo. Hivyo, Mungu kisha huuliza mara moja: “Mnahisi aje wakati wa kuwasili kwa ufalme duniani?” Swali la Mungu lina maana kidogo, lakini huwaacha watu wamekanganyika: “Tunahisi nini? Sisi bado hatujui wakati ambao ufalme utawasili, kwa hiyo tungezungumzaje kuhusu hisia? Zaidi ya hayo, hatuna habari. Kama Ningehisi kitu fulani, kingekuwa ‘kustaajabishwa,’ na siyo kingine zaidi.” Kwa kweli, swali hili si lengo la maneno ya Mungu. Zaidi ya yote, “Wakati Wanangu na watu Wangu wanamiminika katika kiti Changu cha enzi, Naanza rasmi hukumu mbele ya kiti kikuu cheupe cha enzi,” sentensi hii moja inatoa muhtasari wa maendeleo ya ufalme wote wa kiroho. Hakuna anayejua kile ambacho Mungu anataka kufanya katika ufalme wa kiroho wakati wa kipindi hiki, na ni baada tu ya Mungu kutamka maneno haya ndipo kuna kuzinduka kidogo ndani ya watu. Kwa sababu kuna hatua tofauti katika kazi ya Mungu, kazi ya Mungu kote kote katika ulimwengu pia hubadilika. Wakati wa kipindi hiki, Mungu hasa huwaokoa wana na watu wa Mungu, ambako ni kusema, wanapochungwa na malaika, wana na watu wa Mungu huanza kukubali kushughulikiwa na kuvunjwa, wao huanza kwa urasimu kuondoa mawazo na fikira zao, na kuagana na dalili yoyote ya dunia hii; kwa maneno mengine, “hukumu mbele ya kiti kikuu cheupe cha enzi” iliyozungumziwa na Mungu huanza kwa urasimu. Kwa sababu ni hukumu ya Mungu, Mungu lazima atamke sauti Yake—na ingawa maudhui ni tofauti, lengo kila mara huwa lile lile. Leo, kwa kuzingatia toni ambayo kwayo Mungu huzungumza, inaonekana kwamba maneno Yake yanaelekezwa kwa kundi fulani la watu. Kwa kweli, zaidi ya yote, maneno haya hushughulikia asili ya wanadamu wote. Maneno hayo huingia moja kwa moja hadi uti wa mgongo wa mwanadamu, hayaachi kuumiza hisia za mwanadamu, nayo hufichua asili yake yote, bila kuacha chochote, bila kuruhusu chochote kupita. Kuanzia leo, Mungu anafichua kwa urasimu sura ya

kweli ya mwanadamu, na hivyo “huiachilia sauti ya Roho Wangu kwa dunia nzima.” Athari ambayo hutimizwa hatimaye ni “Kupitia maneno Yangu, Nitawasafisha wanadamu na mambo yote miongoni mwa yote yaliyo mbinguni na duniani, ili nchi isiwe chafu na fisadi tena, lakini uwe ufalme mtakatifu.” Maneno haya yanadhihirisha siku za baadaye za ufalme, ambayo yote ni ya ufalme wa Kristo, kama tu alivyosema Mungu, “Yote ni matunda mazuri, wote ni wakulima wenye bidii.” Kwa kawaida, hili litatokea kotekote katika ulimwengu, na halijawekewa mipaka Uchina tu.

Ni wakati tu ambapo Mungu huanza kunena na kutenda ndipo watu humfahamu Yeye kidogo katika dhana zao. Hapo mwanzo, ufahamu huu huwepo tu ndani ya dhana zao, lakini kadiri muda unavyopita, watu huanza kuhisi kwamba mawazo yao wenyewe yanaendelea kutokuwa na manufaa na hayafai; hivyo, wao huja kuamini yote ambayo Mungu husema, kiasi kwamba wao “hutengeneza mahali pa Mungu wa vitendo ndani ya akili zao.” Ni katika akili zao pekee ndipo watu huwa na mahali pa Mungu wa vitendo. Kwa kweli, hata hivyo, hawamjui Mungu, na hunena maneno matupu tu. Ilhali ikifananishwa na zamani, wameendelea vizuri mno—ingawa bado wako mbali sana na Mungu Mwenyewe wa vitendo. Kwa nini Mungu husema kila mara, “Kila siku Natembea miongoni mwa mtiririko usiokoma wa watu, na kila siku Nafanya kazi ndani ya kila mtu”? Kadri ambavyo Mungu husema mambo kama hayo, ndivyo watu wanavyoweza kuyafananisha zaidi na Mungu Mwenyewe wa vitendo wa leo, kwa hiyo wanaweza kumjua vizuri zaidi Mungu wa vitendo kwa kweli. Kwa sababu maneno ya Mungu yananenwa kutoka kwa mtazamo wa mwili, na kutamkwa kwa kutumia lugha ya ubinadamu, watu wanaweza kutambua vyema maneno ya Mungu kwa kuyatathmini dhidi ya vitu yakinifu, na hivyo athari kuu zaidi hutimizwa. Kuongezea, mara kwa mara Mungu hunena kuhusu picha ya “Mimi” ndani ya mioyo ya watu na “Mimi” kwa kweli, ambalo huwafanya watu wawe radhi zaidi kusafisha picha ya Mungu ndani ya mioyo yao, na hivyo kuwa radhi kujua na kufungamana na Mungu Mwenyewe wa vitendo. Hii ni hekima ya maneno ya Mungu. Kadri ambavyo Mungu husema mambo kama hayo, ndivyo faida kwa ufahamu wa watu kuhusu Mungu huwa kuu zaidi, na hivyo Mungu husema, “Nisingekuwa mwili, mwanadamu hangewahi kunijua, na hata angekuja kunijua, je, si maarifa kama hayo bado yangekuwa dhana?” Kweli, kama watu wangehitajika kumjua Mungu kufuatana na dhana zao wenyewe, ingekuwa rahisi kwao, wangeburudika na kufurahi, na hivyo Mungu hangekuwa dhahiri daima, na asiye wa vitendo katika mioyo ya watu, ambalo lingethibitisha kwamba Shetani, na si Mungu, anashikilia utawala juu ya ulimwengu wote; hivyo, maneno ya Mungu kwamba “Nimerejesha mamlaka Yangu” yangesalia matupu daima.

Wakati ambapo uungu huanza kutenda moja kwa moja ni wakati ambao pia ufalme hushuka kwa urasimu kwa ulimwengu wa mwanadamu. Lakini kile ambacho husemwa hapa ni kwamba

ufalme hushuka miongoni mwa binadamu, siyo kwamba ufalme huanza kuonekana polepole miongoni mwa wanadamu—na hivyo kile kinachozungumziwa leo ni ujenzi wa ufalme, na siyo jinsi unavyoanza kuonekana. Mbona Mungu husema kila mara, “Mambo yote yanakimya” Yawezekana kwamba mambo yote yanasimama kabisa? Yawezekana kwamba milima mikubwa inakimya kwa kweli? Kwa hiyo mbona watu hawana ufahamu wa hili? Yawezekana kwamba neno la Mungu lina makosa? Au Mungu anatia chumvi? Kwa sababu kila kitu ambacho Mungu hufanya hutekelezwa katika mazingira fulani, hakuna ambaye hukifahamu, au ambaye ana uwezo wa kukiona kwa macho yake mwenyewe, na yote ambayo watu wanaweza kufanya tu ni kumsikiliza Mungu akinena. Kwa sababu ya uadhama ambao Mungu hutenda, wakati ambapo Mungu hufika, ni kana kwamba kumekuwa na mabadiliko makubwa mno mbinguni na duniani; na kwa Mungu, huonekana kwamba wote wanatazama wakati huu. Leo, ukweli bado haujafika. Watu wamejifunza kidogo tu kutoka kwa sehemu ya maana halisi ya maneno ya Mungu. Maana ya kweli inangoja wakati ambao watajisaifisha na dhana zao; wakati huo tu ndipo watakuwa na fahamu ya kile ambacho Mungu mwenye mwili anafanya duniani na mbinguni leo. Ndani ya watu wa Mungu Uchina hakuna tu sumu ya joka kubwa jekundu. Hiyo, pia, ndiyo asili ya joka kubwa jekundu iliyofichuliwa kwa wingi zaidi, na kwa dhahiri zaidi, ndani yao. Lakini Mungu hazungumzi kuhusu hili moja kwa moja, Akitaja tu kidogo kuhusu sumu ya joka kubwa jekundu. Kwa njia hii, Hayafichui makovu ya mwanadamu moja kwa moja, ambalo ni la manufaa zaidi kwa maendeleo ya mwanadamu. Watoto wa joka kubwa jekundu hawapendi kuitwa ukoo wa joka kubwa jekundu mbele ya wengine. Ni kana kwamba maneno “joka kubwa jekundu” huleta aibu kwao; hakuna yeyote kati yao aliye radhi kuzungumza kuhusu maneno haya, na hivyo Mungu husema tu, “hatua hii ya kazi Yangu hasa inawaangazia, na hiki ni kipengele kimoja cha umuhimu wa kupata mwili Kwangu Uchina.” Kwa usahihi zaidi, Mungu amekuja hasa kuwashinda wawakilishi wa kiumboasili wa watoto wa joka kubwa jekundu, ambalo ni umuhimu wa kupata mwili kwa Mungu Uchina.

“Nijapo binafsi miongoni mwa binadamu, malaika wanaanza kazi ya uchungaji wakati huo huo.” Kwa kweli, haichukuliwi neno kwa neno kwamba Roho wa Mungu huwasili tu katika ulimwengu wa mwanadamu wakati ambapo malaika huanza kazi yao miongoni mwa watu wote. Badala yake, sehemu hizi mbili za kazi—kazi ya uungu na uchungaji wa malaika—hutekelezwa sawia. Linalofuata, Mungu huzungumza kidogo kuhusu uchungaji wa malaika. Wakati ambapo Yeye husema kwamba “wana na watu wote hawapati tu majaribio na uchungaji, lakini wanaweza pia kuona, na macho yao wenyewe, tukio la kila aina za maono,” watu wengi sana huwa na mawazo tele kuhusu neno “maono.” Maono yanahusu matukio ya rohoni katika mawazo ya watu. Lakini yaliyomo katika kazi husalia ufahamu wa Mungu Mwenyewe wa vitendo. Maono ni njia ambayo kwayo malaika hufanya kazi. Yanaweza kuwapa watu hisia au ndoto,

yakiwakubalia kutambua kuweko kwa malaika. Lakini malaika husalia wasioonekana kwa mwanadamu. Mbinu ambayo kwayo wao hufanya kazi miongoni mwa wana na watu wa Mungu ni kuwapa nuru na kuwaangaza moja kwa moja, kuongezea kwayo ni kuwashughulikia na kuwavunja. Wao hutoa mahubiri mara chache. Kwa kawaida, mawasiliano kati ya watu ni jambo la pekee; hili ndilo linalofanyika katika mataifa nje ya Uchina. Ndani ya maneno ya Mungu kuna ufunuo wa hali za kuishi za wanadamu wote—kwa kawaida, hili linaelekezwa hasa kwa watoto wa joka kubwa jekundu. Kati ya hali mbalimbali za kiroho za wanadamu wote, Mungu huteua zile ambazo ni za uwakilishi ili zitumike kama mifano. Hivyo, maneno ya Mungu huwavua watu wakawa uchi, na hawaoni aibu yoyote, ama sivyo hawana muda wa kujificha kutoka kwa nuru iangazayo, na wao hushindwa katika ujanja wao. Tabia nyingi za mwanadamu ni picha nyingi kupita kiasi, ambazo Mungu amechora kutoka nyakati za kale mpaka leo, na ambazo Atachora kutoka leo mpaka kesho. Yote ambayo Yeye huchora ni ubaya wa mwanadamu: Wengine hutokwa na machozi gizani, inavyoonekana kwa nje wao husikitishwa kwa ajili ya kutoona tena, wengine hucheka, wengine hupigwa kwa nguvu na mawimbi makubwa, wengine hutembea juu ya barabara za mlima zinazoinuka na kushuka, wengine hutafuta katikati ya nyika kubwa mno, wakitetemeka kwa woga, kama ndege aliyegutushwa na mlilo tu wa uzi wa uta, wakitishwa kabisa na kuliwa na wanyama wa mwitu katika milima. Mikononi mwa Mungu, hizi tabia nyingi mbaya hugeuka kuwa za kugusa, uwakilishaji wa picha kama za maisha, nyingi ya hizo za kutisha sana kutazama, la sivyo za kiasi cha kutosha kuwaogofya watu na kuwaacha waliokanganyikiwa na kutatanishwa. Machoni pa Mungu, vyote vinavyoonyeshwa ndani ya mwanadamu ni ubaya tu, na hata ingawa kinaweza kuchochea huruma, bado ni ubaya. Sehemu maalum ya tofauti kati ya mwanadamu na Mungu ni kwamba udhaifu wa mwanadamu upo katika mwelekeo wake wa kuonyesha ukarimu wake kuelekea wengine. Mungu, hata hivyo, Amekuwa yule yule kila mara kwa mwanadamu, ambalo lina maana kwamba Yeye kila mara Amekuwa na mtazamo ule ule. Yeye kila mara si mkarimu jinsi watu hufikiria, kama mama mwenye tajiriba ambaye watoto wake kila mara huwa katika sehemu ya mbele kabisa ya mawazo yake. Kwa kweli, kama Mungu hangetaka kutumia mbinu nyingi ili kulishinda joka kubwa jekundu, hakuna vile ambavyo Angejisalimisha kwa aibu kama hiyo, Akijiruhusu kutiishwa chini ya udhaifu wa mwanadamu. Kulingana na tabia ya Mungu, yote ambayo watu hufanya na kusema huchochea ghadhabu ya Mungu, na wao wanapaswa kuadibiwa. hina ni taifa la joka kubwa jekundu, na nchi ambayo kwayo Mungu mwenye mwili huishi, Mungu lazima amezee hasira Yake na kuwashinda watoto wote wa joka kubwa jekundu; ilhali Yeye kila mara Atawachukia sana watoto wa joka kubwa jekundu, yaani, Yeye kila mara Atayachukia sana yote ambayo hutoka kwa joka kubwa jekundu—na hili halitabadilika kamwe.

Hakuna ambaye amewahi kufahamu matendo yoyote ya Mungu, wala matendo Yake

hayajawahi kutazamwa na chochote. Wakati ambapo Mungu alirudi Sayuni, kwa mfano, ni nani aliyefahamu hili? Hivyo, maneno kama “Naja polepole miongoni mwa wanadamu, na Naondoka taratibu. Kuna yeyote aliyewahi kuniona?” yanaonyesha kwamba mwanadamu kweli hukosa welekevu wa kukubali matukio ya ufalme wa kiroho. Zamani, Mungu alisema kwamba “jua ni la joto, mwezi ni wa mng’aro” wakati wa kurudi Kwake Sayuni. Kwa sababu watu bado wameshughulishwa na kurudi kwa Mungu Zayuni—kwa sababu bado hawajaliacha—Mungu hutamka moja kwa moja maneno “jua ni la joto, na mwezi ni wa mng’aro” ili kupatana na dhana za watu. Kutokana na hilo, wakati ambapo dhana za watu hugongwa na maneno ya Mungu, wao huona kwamba matendo ya Mungu ni ya ajabu sana, na huona kwamba maneno Yake ni ya maana sana na yasiyoweza kueleweka, na yasiyotambulikana kwa wote; hivyo, wao huliweka jambo hili pembeni kabisa, na kuhisi ubayana kidogo ndani ya roho zao, kana kwamba Mungu amerudi Sayuni tayari, na kwa hiyo watu hawazingatii sana jambo hili. Kuanzia wakati huo kuendelea, wao hukubali maneno ya Mungu kwa moyo mmoja na fikira moja, na hawawi na wasiwasi tena kwamba watafikwa na msiba mkuu baada ya kurudi kwa Mungu Sayuni. Ni wakati huo tu ndiyo huwa rahisi kwa watu kuyakubali maneno ya Mungu, kulenga zingatiao lao lote kwa maneno ya Mungu, wakiachwa bila hamu ya kufikiria jambo lingine lolote.

Nyongeza: Sura ya 2

Watu wanapomwona Mungu wa vitendo, wanapoishi maisha yao binafsi na, wanapotembea sako kwa bako na, na wanapoishi na Mungu Mwenyewe, wao huweka kando udadisi ambao umekuwa ndani ya mioyo yao kwa miaka mingi sana. Ufahamu wa Mungu uliozungumziwa awali ni hatua ya kwanza tu; ingawa watu wana ufahamu wa Mungu, bado kuna mashaka mengi ya kuchagiza ndani ya mioyo yao: Mungu alitoka wapi? Je, Mungu hula? Mungu yuko tofauti sana na watu wa kawaida? Kwa Mungu, kushughulikia watu wote ni jambo la uhakika, kazi rahisi tu? Je, yote yanayonenwa kutoka kwa kinywa cha Mungu ni siri za mbinguni? Je, yote Asemayo ni makubwa zaidi kuliko yale ya viumbe vyote vilivyoundwa? Je, nuru hung’aa kutoka kwa macho ya Mungu? Na kadhalika—dhana za watu zinaweza kufanya hili. Mambo haya ndiyo mnayopaswa kuelewa na kuingia ndani kabla ya mengine yote. Katika dhana za watu, Mungu aliyepata mwili bado ni Mungu asiye dhahiri. Isingekuwa kupitia kwa ufahamu wa vitendo, watu wasingeweza kamwe kunieleva, na wasingeaona kamwe matendo Yangu katika uzoefu wao. Ni kwa sababu tu Nilipata mwili ndiyo maana watu “hawawezi kuelewa” mapenzi Yangu. Kama Singekuwa Nimepata mwili, na Ngingekuwa bado mbinguni, bado katika ulimwengu wa kiroho, basi watu “wangenijua,” wangeinama na kuniabudu, na wangezungeza kuhusu wao “kunifahamu” kupitia kwa uzoefu wao—lakini ufahamu kama huo ungekuwa na maana gani? Thamani yake kama kumbukumbu ingekuwa gani? Je, ufahamu unaotokana na dhana za watu ungekuwa halisi? Sitaki ufahamu wa akili za watu—Nataka ufahamu wa vitendo.

Mapenzi Yangu hufichuliwa miongoni mwenu nyakati zote, na nyakati zote huwa kuna mwangaza Wangu na kupata nuru. Na Ninapotenda moja kwa moja katika uungu, halichujwi kupitia kwa akili, hakuna haja ya kuongeza “viungo”—hili ni tendo nyoofo la uungu. Watu wanaweza kufanya nini? Je, yote tangu wakati wa uumbaji mpaka leo hayajatekelezwa binafsi na Mimi? Wakati uliopita, Nilizungumza kuhusu Roho aliyeongezwa nguvu mara saba, lakini hakuna mtu aliyeweza kufahamu kiini Chake—hata walipokijua, hawakuweza kufahamu kabisa. Wakati ambapo Nafanya kazi katika ubinadamu kwa kuongozwa na uungu, kwa kuwa kazi hii inatekelezwa katika hali ambazo watu wanaamini si za mwujiza bali za kawaida, inatajwa kuwa kazi ya Roho Mtakatifu. Ninapofanya kazi moja kwa moja katika uungu, kwa vile Sizuiwi na dhana za watu, na Sipaswi kutii mipaka ya “mwujiza” katika dhana zao, kazi hii ina matokeo ya mara moja, inaelekea kwa kiini cha jambo, inagonga ndipo. Kutokana na hilo, hatua hii ya kazi ni takatifu zaidi, ni ya haraka mara mbili, ufahamu wa watu umechapuka, na maneno Yangu yanaongezeka, kusababisha watu wote kuharakisha kuyafikia. Kwa kuwa matokeo ni tofauti, kwa kuwa njia, asili, na maudhui ya kazi Yangu si sawa—na, zaidi ya hayo, kwa kuwa Nimeanza kufanya kazi rasmi katika mwili, kwa kuzingatia yaliyotangulia, hatua hii ya kazi inatajwa kama kazi ya Roho aliyeongezwa nguvu mara saba. Si kitu dhahania. Kufuatia maendeleo katika njia ambayo kwayo Nafanya kazi ndani yenu, na kufuatia majilio ya ufalme, Roho aliyeongezwa nguvu mara saba anaanza kufanya kazi, na kazi hii daima hupanuka zaidi na kuwa na nguvu zaidi. Watu wote wanapomwona Mungu na wote waone kwamba Roho wa Mungu yuko miongoni mwa wanadamu, umuhimu kamili wa kupata mwili Kwangu huwa dhahiri. Hakuna haja ya kufupisha—watu wanalijua hili kwa kawaida.

Kuzingatia hali nyingi—mbinu ambazo kwazo Nafanya kazi, hatua za kazi Yangu, sauti ya maneno Yangu leo, na kadhalika—yanayotoka kinywani Mwangu sasa pekee ndiyo “matamko ya Roho saba” Katika hali ya kweli. Ingawa Nilizungumza pia wakati uliopita, huo ulikuwa wakati wa hatua ya ujenzi wa kanisa. Lilikuwa kama dibaji na faharasa katika riwaya—halikuwa na kiini; ni matamko ya leo pekee ndiyo yanaweza kuitwa kiini cha matamko ya Roho saba. “Matamko ya Roho saba” yanahusu matamko yanayotoka kwa kiti cha enzi, ambalo ni kusema, yanatamkwa moja kwa moja katika uungu. Wakati ambapo matamko Yangu yaligeuka kufichua siri za mbinguni ulikuwa wakati ambapo Nilizungumza moja kwa moja katika uungu. Kwa maneno mengine, bila kuzuiwa na ubinadamu, Nilifichua moja kwa moja siri na hali zote za ulimwengu wa kiroho. Kwa nini Nasema kwamba hapo awali Nilipaswa kutii mipaka ya ubinadamu? Hili linahitaji ufafanuzi. Machoni pa watu, hakuna mtu anayeweza kufichua siri za mbinguni; isingekuwa Mungu Mwenyewe, hakuna mtu mwingine duniani angeweza kujua siri hizi. Hivyo, Nazungumzia dhana za watu na Nasema kwamba zamani Sikufichua siri zozote kwa sababu Nilipaswa kutii mipaka ya ubinadamu. Kwa ubayana zaidi, hata hivyo, huu si ukweli:

Maudhui ya maneno Yangu hutofautiana kama vile kazi Yangu hutofautiana, na hivyo, wakati ambapo Nilianza kutekeleza huduma Yangu katika uungu, Nilifichua siri; zamani, ilinibidi Nifanye kazi katika hali ambazo watu wote waliziona kuwa kawaida, na maneno Niliyonena yalikuwa na uwezo wa kutimizwa katika dhana za watu. Nilipoanza kufichua siri, hakuna hata moja ya hizi iliyofikiwa na dhana za watu—hazikuwa kama fikira za binadamu. Kwa hiyo, Nilianza rasmi kugeukia unenaji katika uungu, na haya yalikuwa matamko ya Roho saba katika hali ya kweli. Ingawa maneno ya zamani yalikuwa matamko kutoka kwa kiti cha enzi, yalinenwa kwa msingi wa kile kilichoweza kufikiwa na watu, na hivyo hayakutamkwa moja kwa moja katika uungu—kwa sababu hiyo hayakuwa matamko ya Roho saba katika hali ya kweli.

Sura ya 12

Watu wote wanapotilia maanani, wakati vitu vyote vinafanywa upya na kuhuishwa, wakati kila mtu anamtii Mungu bila shaka, na yuko tayari kubeba jukumu zito la mzigo wa Mungu—hapa ndipo wakati umeme wa mashariki unatoka, ukiangaza yote kutoka Mashariki hadi Magharibi, ukiyatisha yote ya ulimwengu na ujaji wa mwanga huu; na wakati huu, Mungu tena huanza maisha Yake mapya. Ambayo ni kusema, wakati huu Mungu huanza kazi mpya duniani, akitangaza kwa watu wa ulimwengu wote kwamba “Wakati umeme unatoka Mashariki—ambao pia ni wakati hasa Naanza kutamka maneno Yangu—umeme unapotoka, mbingu yote inaangazwa, na mabadiliko yanatokea kwenye nyota zote.” Hivyo, ni wakati upi ambao umeme unatoka kutoka Mashariki? Wakati mbingu zinatiwa giza na dunia inapunguka mwanga pia ni wakati ambapo Mungu huuficha uso Wake kutoka kwa dunia, na wakati hasa ambapo yote chini ya mbingu yako karibu kuzongwa na dhoruba kuu. Wakati huu, watu wote wanaingwa na hofu kubwa, wakiogopa radi, wakiogopa kung’aa kwa umeme, na hata kuogopa zaidi shambulio la gharika, kiasi kwamba wengi wao wanafumba macho na kusubiri Mungu aachilie huru ghadhabu Yake na kuwabwaga. Na hali mbalimbali zinapoendelea kupita, umeme wa mashariki unatoka ghafla. Ambayo ni kusema, katika Mashariki ya dunia, kutoka wakati ushuhuda kwa Mungu Mwenyewe huanza, hadi wakati Yeye huanza kufanya kazi, mpaka wakati uungu huanza kushika madaraka makuu pande zote duniani—huu ni mwale unaong’aa wa umeme wa mashariki, ambao daima umemulika kwa ulimwengu mzima. Wakati ambapo nchi duniani zinakuwa ulimwengu wa Kristo ndio wakati ambapo ulimwengu mzima unatiwa nuru. Sasa ndio wakati ambapo umeme wa mashariki unatoka: Mungu mwenye mwili Anaanza kufanya kazi, na, zaidi ya hayo, Anaongea moja kwa moja katika uungu. Inaweza kusemwa kwamba Mungu anapoanza kuongea duniani ni wakati ambapo umeme wa mashariki unatoka. Kwa usahihi zaidi, wakati ambapo maji ya uhai yanatiririka kutoka katika kiti cha enzi—wakati ambapo matamshi kutoka katika kiti cha enzi huanza—bila shaka ni wakati ambapo matamshi ya Roho saba huanza kirasmi. Wakati huu, umeme wa mashariki unaanza kutoa nje, na kwa sababu ya kipindi chake, kiwango cha

mwangaza pia kinabadilika, na kunao, pia, mpaka kwa mawanda ya nuru. Lakini kadri kazi ya Mungu inavyoendelea, kadri mpango Wake unavyobadilika—kadri kazi kwa wana na watu wa Mungu inavyobadilika—umeme unazidi kutekeleza kazi yake ya asili, kiasi kwamba yote kote duniani yanaangazwa, na hakuna mashapo ama takataka zinazobaki. Huu ndio udhihirisho wa mpango wa Mungu wa usimamizi wa miaka 6000, na tunda hasa linalofurahiwa na Mungu. “Nyota” haihusu nyota zilizo angani, lakini wana na watu wote wa Mungu ambao hufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Kwa sababu wana shuhudia kwa Mungu katika ufalme wa Mungu, na kumwakilisha Mungu katika ufalme wa Mungu, na kwa sababu wao ni viumbe, wanaitwa “nyota.” “Kubadilika” kunahusu mabadiliko katika utambulisho na hadhi: Yanabadilika kutoka kwa watu duniani hadi kwa watu wa ufalme, na, zaidi ya hayo, Mungu yuko pamoja nao, na utukufu wa Mungu uko ndani yao. Kwa hiyo, wanashika mamlaka ya kifalme badala ya Mungu, na sumu na najisi ndani yao zinatakaswa kwa sababu ya kazi ya Mungu, hatimaye zikiwafanya kufaa kwa matumizi na Mungu na kuupendeza moyo wa Mungu—ambacho ni kipengele kimoja cha maana cha maneno haya. Wakati ambapo mwale wa mwanga kutoka kwa Mungu unaiangaza nchi yote, vitu vyote mbinguni na duniani vitabadilika kwa viwango mbalimbali, na nyota angani pia zitabadilika, jua na mwezi vitafanywa upya, na watu duniani watafanywa upya baadaye—ambayo yote ni kazi inayofanywa na Mungu katikati ya mbingu na dunia, na haishangazi.

Mungu anapowaokoa watu—ambayo, kwa kawaida, haijumuishi wale ambao si wateule—ni wakati hasa ambapo Mungu huwatakaswa na kuwahukumu watu, na watu wote hulika kwa uchungu, ama kuanguka vitandani mwao, au wanabwagwa na kutumbukizwa katika jahanamu ya kifo kwa sababu ya maneno ya Mungu. Ni kwa sababu tu ya matamshi ya Mungu kwamba wanaanza kujijua. Kama sio, macho yao yangekuwa ya chura—yakiangalia juu, hakuna anayesadiki, hakuna kati yao akijijua, bila kujua uzito wao. Kwa kweli watu wamepotoshwa na Shetani kwa kiwango kikubwa. Ni kwa sababu hasa ya kudura ya Mungu kwamba uso mbaya wa mwanadamu unaelezwa waziwazi kabisa, ukimsababisha mwanadamu, baada ya kuuona, kuulinganisha na uso wake mwenyewe wa kweli. Watu wote wanajua kwamba idadi ya seli za ubongo walizo nazo vichwani mwao zinaonekana kuwa wazi kabisa kwa Mungu, sembuse nyuso zao mbaya au mawazo ya ndani kabisa. Kwa maneno ya “Wanadamu wote wanakuwa kana kwamba wamepangwa vizuri. Chini ya mng’aro wa mwale huu wa mwangaza kutoka Mashariki, wanadamu wote wanafichuliwa katika maumbo yao ya asili, macho yao yaking’aa, wakikosa uhakika wa kile wanachopsawa kufanya” inaweza kuonekana kwamba siku moja kazi ya Mungu iishapo, wanadamu wote watakuwa wamehukumiwa na Mungu. Hakuna atakayeweza kutoroka, Mungu atashughulika na watu wote mmoja mmoja, Asikose kutilia maanani hata mmoja wao, na hapo tu ndipo Moyo wa Mungu utaridhika. Na hivyo, Mungu anasema, “Wao pia ni kama

wanyama wanaoitoroka kutoka kwa mwangaza Wangu amabao wanakimbilia usalama katika mapango ya milimani—ilhali, hakuna hata mmoja kati yao anayeweza kufutiliwa mbali kutoka katika mwanga Wangu.” Watu ni wanyama duni na wa hali ya chini. Wakiishi mikononi mwa Shetani, ni kana kwamba wamepata usalama katika misitu ya kale ndani sana ya milima—lakini kwa sababu vitu vyote haviwezi kutoroka uchomaji kwa mwako wa moto wa Mungu, hata vikiwa chini ya “ulinzi” wa nguvu za Shetani, vingewezaje kusahaulika na Mungu?

Wanapokubali kuwasili kwa maneno ya Mungu, maumbo mbalimbali yasiyo ya kawaida na hali za ajabu za watu wote zinaonyeshwa kwa mchoro wa kalamu ya wino ya Mungu; Mungu huzungumza ifaavyo mahitaji na akili ya mwanadamu. Hivyo, kwa watu, Mungu anaonekana kuwa mjuzi mzuri katika saikolojia. Ni kana kwamba Mungu ni mtaalamu wa mambo ya saikolojia, lakini pia kana kwamba Mungu ni mtaalamu wa tiba ya sehemu za ndani za mwili—haishangazi kwamba Ana ufahamu kama huo wa mwanadamu, ambaye ni “mgumu kufahamika”. Kadri watu wanavyofikiria hili, ndivyo hisia yao ya thamani ya Mungu inavyokuwa kubwa zaidi, na ndivyo wanavyohisi zaidi kwamba Mungu ni mkubwa na asiyeleweka. Ni kana kwamba, kati ya mwanadamu na Mungu, kuna mpaka usiovukika wa mbingu, lakini pia kana kwamba hao wawili wanaangaliana kutoka kingo mkabala za Mto Chu,^[a] kila mmoja asiweze kufanya kingine zaidi ya kumtazama mwingine. Ambayo ni kusema, watu wa dunia humtazama Mungu tu kwa macho yao, hawajawahi kuwa na fursa ya kumchunguza kwa karibu, na yote waliyo nayo ni hisia ya upendo. Katika mioyo yao, daima wana hisia kwamba Mungu anapendeza, lakini kwa sababu Mungu ni “mkatili mno na asiye na huruma”, hawajawahi kuwa na fursa ya kuzungumzia maumivu makali katika mioyo yao mbele Yake. Wao ni kama mke mzuri mchanga mbele ya mume wake—ambaye, kwa sababu ya uaminifu wa mume wake, hajawahi kuwa na nafasi ya kutoa wazi hisia zake za kweli. Watu ni mafidhuli wanaojidharau, na hivyo, kwa sababu ya udhaifu wao, kwa sababu ya kukosa kwao kujiheshimu, chuki Yangu ya mwanadamu kwa kiasi fulani inaongezeka bila kufahamu, na ghadhabu katika moyo Wangu inatoka nje kwa nguvu. Katika akili Yangu, ni kana kwamba nimepitia kiwewe. Nilipoteza matumaini kwa mwanadamu kitambo, lakini kwa sababu “Kwa mara nyingine, siku Yangu inaikaribia jamii ya binadamu, mara nyingine ikiiamsha jamii ya binadamu, ikiwapa binadamu hatua ambayo kwayo inafaa kutengeneza mwanzo mpya,” mara nyingine Ninakusanya ujasiri kuwashinda wanadamu wote, kumteka na kumshinda joka kuu jekundu. Kusudi la asili la Mungu lilikuwa kama ifuatavyo: kutofanya chochote zaidi ya kuwashinda wazao wa joka kuu jekundu katika China; hili tu ndilo lingeweza kufikiriwa kuwa kuzidiwa nguvu kwa joka kuu jekundu, ushinde wa joka kuu jekundu, na hili tu ndilo lingetosha kudhibitisha kwamba Mungu hutawala kama Mfalme duniani kote, ikidhibitisha utimilifu wa shughuli kuu ya Mungu, na kwamba Mungu ana mwanzo mpya duniani, na Anatukuzwa duniani. Kwa sababu ya mandhari mazuri ya mwisho, Mungu hana budi kuonyesha uchu ulio ndani ya moyo Wake: “Moyo Wangu

unapiga na, kufuatia mdundo wa mpigo wa moyo Wangu, milima inaruka kwa furaha, maji yanacheza kwa furaha, na mawimbi, kwa wakati ufaao, yanagonga juu ya mawe ya mwamba. Ni vigumu kueleza kile kilicho ndani ya moyo Wangu.” Kutoka kwa hili inaweza kuonekana kwamba kile kilichopangwa na Mungu ni kile ambacho Mungu ameshatimiza, kwamba kilijaaliwa na Mungu, na ni kile hasa Mungu huwafanya watu kupitia na kutazama. Mandhari ya ufalme ni mazuri, Mfalme wa ufalme ni mshindi, kutoka kichwani hadi kidoleni hakuna dalili yoyote ya mwili na damu, Yeye mzima ni mtakatifu. Mwili wake wote unang’aa kwa utukufu mtakatifu, haujatiwa doa na mawazo ya kibinadamu hata kidogo, mwili Wake wote, kutoka juu hadi chini, umejaa haki na uzuri wa mbingu, na unatoa harufu nzuri ya kupendeza mno. Kama wapenzi katika Wimbo wa Suleiman, Yeye bado ni mzuri kuliko watakatifu wote, wa juu zaidi kuliko watakatifu wa kale, Yeye ni mfano kati ya watu wote, na Asiyelinganishika na mwanadamu; watu hawafai kumtazama moja kwa moja. Hakuna awezaye kuufikia uso mtukufu wa Mungu, sura ya Mungu, au taswira ya Mungu, hakuna awezaye kushindana, na hakuna awezaye kuyasifu kwa urahisi kwa kinywa chake.

Maneno ya Mungu hayana mwisho, kama maji yabubujikayo kutoka kwa chemchemi hayatawahi kukauka, na hivyo hakuna awezaye kuelewa siri ya mpango wa Mungu wa usimamizi—lakini kwa Mungu, siri kama hizo haziishi. Akitumia njia na lugha tofauti, Mungu amezungumza mara nyingi kuhusu kufanywa Kwake upya na kutamka kubadilishwa kabisa kwa ulimwengu mzima, kila wakati ukiwa wa kina zaidi kuliko wakati uliopita: “Nataka vitu vyote visivyo safi vichomeke na kuwa jivu Nikitazama, Nataka wana wote wa kutotii wapotee kutoka mbele ya macho Yangu, wasikawie tena katika uwepo.” Kwa nini Mungu husema mambo kama hayo tena na tena? Je, Haogopi watu watachoshwa nayo? Watu wanapapasa tu katikati ya maneno ya Mungu, wakitaka kumjua Mungu kwa njia hii, lakini kamwe hawakumbuki kujichunguza. Hivyo, Mungu hutumia njia hizi kuwakumbusha, kuwafanya wajijue, ili kutoka kwao wenyewe wanaweza kupata kujua uasi wa mwanadamu, na hivyo kufuta uasi wao mbele za Mungu. Wanaposoma kwamba Mungu anataka “kusafisha na kutatua,” hali yao ya moyo inakua na wasiwasi mara moja, na misuli yao, pia, inaonekana kuacha kusonga. Mara moja wanarudi mbele za Mungu kujikosoa, na hivyo wanakuja kumjua Mungu. Baada ya hili—baada ya wao kuamua—Mungu hutumia fursa hiyo kuwaonyesha kiini cha joka kuu jekundu; hivyo, watu hushiriki na ufalme wa kiroho moja kwa moja, na kwa sababu ya wajibu unaochukuliwa na uamuzi wao, akili zao zinaanza pia kuchukua wajibu fulani, ambalo linazidisha pendo kati ya mwanadamu na Mungu—ambalo ni la manufaa muhimu zaidi kwa kazi ya Mungu katika mwili. Kwa njia hii, watu hutaka kukumbuka nyakati zilizopita bila kufahamu: Katika wakati uliopita, kwa miaka watu walimwamini Mungu asiye yakini, kwa miaka kamwe hawakuwekwa huru mioyoni mwao, hawakuwa na uwezo wa raha kuu, na ingawa walimwamini Mungu, hakukuwa

na mpango katika maisha yao. Ilikuwa kana kwamba hakukuwa na tofauti na kabla ya wao kuwa waumini, maisha yao bado yalihisi kuwa matupu na yasiyo na matumaini, ilikuwa kana kwamba imani yao wakati huo ilikuwa aina ya mtego, na kana kwamba ingekuwa heri wasingeamini. Kwa sababu walimtazama Mungu Mwenyewe wa vitendo wa leo, ni kana kwamba mbingu na dunia zimefanywa upya; maisha yao yameng'aa, hawako bila matumaini tena, na kwa sababu ya ujaji wa Mungu wa vitendo, wanahisi kuwa imara katika mioyo yao na watulivu ndani ya roho zao. Hawafuatilii upepo tena na kushikia yasiyo dhahiri katika yote wafanyayo, ufuatiliaji wao haukosi lengo maalum tena na hawatupi mikono huku na kule ovyo ovyo tena. Maisha ya leo ni mazuri hata zaidi, watu wameingia katika ufalme bila kutarajia na kuwa mmoja wa watu wa Mungu, na baadaye.... Katika mioyo yao, watu wanavyofikiria zaidi, ndivyo utamu unavyokuwa mkuu zaidi, wanavyofikiria zaidi, ndivyo wanavyokuwa na furaha zaidi, na ndivyo wanavyotiwa moyo zaidi kumpenda Mungu. Hivyo, bila wao kutambua, urafiki kati ya Mungu na mwanadamu unaimarishwa. Watu wanampenda Mungu zaidi, na kumjua Mungu zaidi, na kazi ya Mungu ndani ya mwanadamu inazidi kuwa rahisi, na haiwalazimishi au kuwashurutisha watu tena, lakini inafuata hali ya asili ya maisha, na mwanadamu hutekeleza kazi yake maalum—hapo tu ndipo wataweza kumjua Mungu polepole. Hii tu ndiyo hekima ya Mungu—haijumuishi juhudi hata kidogo, na inazalishwa kama ifaavyo asili ya mwanadamu. Hivyo, wakati huu Mungu anasema, “Katika wakati wa kupata mwili Kwangu katika dunia ya binadamu, binadamu walifika pasipo kujua katika siku hii na usaidizi wa uongozi wa mkono Wangu, pasipo kujua wakaja kunifahamu. Lakini, kuhusu jinsi ya kutembea katika njia iliyo mbele, hakuna aliye na fununu, hakuna anayejua, na bado hakuna aliye na kidokezo juu ya mwelekeo ambao hiyo njia itampeleka. Mwenyezi pekee akimwangalia ndipo yeyote ataweza kutembea njia hiyo hadi mwisho; akiongozwa tu na umeme kutoka Mashariki ndipo yeyote ataweza kuvuka kizingiti kinachoelekea katika ufalme Wangu.” Je, huu si muhtasari wa kile Nimeeleza katika moyo wa mwanadamu hapo juu? Hii ndiyo siri ya maneno ya Mungu. Kile ambacho mwanadamu anafikiria moyoni mwake ni hasa kile ambacho Mungu ananena kwa kinywa Chake, na kile Mungu anachonena kwa kinywa Chake ndicho hasa tamanio la mwanadamu. Hapa hasa ndipo Mungu ni bingwa zaidi kwacho katika kuufichua moyo wa mwanadamu; kama sivyo, wote wangetolewa shaka kwa dhati vipi? Je, haya si matokeo Mungu anataka kutimiza katika kumshinda joka kuu jekundu?

Kwa kweli, kama lilivyokuwa kusudi la asili la Mungu, maana ya maneno Yake mengi haiko katika maana yake ya juu juu. Katika maneno Yake mengi, Mungu anabadilisha dhana za watu kwa kusudi tu na kuvuta kwingine uangalifu wao. Mungu hashikizi umuhimu wowote kwa maneno haya, na hivyo maneno mengi hayastahili ufafanuzi. Wakati ushindi wa mwanadamu kwa maneno ya Mungu umefika mahali upo leo, nguvu ya watu imefika mahali fulani, na hivyo

Mungu baadaye hutamka maneno zaidi ya onyo—katiba Atoayo kwa watu wa Mungu: “Ingawa wanadamu ambao wanaijaza dunia ni wengi kama nyota, Nawajua wote wazi kama Ninavyotazama kiganja cha mkono Wangu mwenyewe. Na, ingawa wanadamu ambao ‘wananipenda’ ni wengi pia kama mchanga wa bahari, ni wachache tu ndio waliochaguliwa na Mimi: wale tu wanaoufuatilia mwanga unaong’aa, walio kando na wale ‘wanaonipenda’.” Kwa kweli, kunao wengi wasemao wanampenda Mungu, lakini kunao wachache wanaompenda katika mioyo yao—ambayo, ingeonekana, inaweza kujulikana wazi hata macho yakiwa yamefumbwa. Hii ndiyo hali halisi ya dunia nzima ya wale wamwaminio Mungu. Katika hili, tunaona kwamba sasa Mungu amegeuza kazi yake kuwa ile ya “kuwaainisha watu”, ambayo inaonyesha kwamba kile Mungu hutaka, na kile kinachomridhisha Mungu, si kanisa la leo, lakini ni ufalme baada ya uainishaji. Kwa sasa, Anatoa onyo zaidi kwa “bidhaa hatari” zote: Isipokuwa Mungu asichukue hatua, punde tu Mungu anapoanza kuchukua hatua, watu hawa watafutwa kutoka katika ufalme. Mungu kamwe hafanyi mambo bila uangalifu, daima Yeye hutenda kulingana na kanuni ya “moja ni moja na mbili ni mbili,” na kama kuna wale ambao Hataki kuwatazama, Yeye hufanya kila Awezalo kuwafuta ili kuwakomesha kusababisha taabu baadaye. Hili linaitwa “kuondoa taka na kusafisha kabisa.” Wakati Mungu anatangaza amri za kiutawala kwa mwanadamu ndio wakati hasa ambapo Anaonyesha matendo yake ya muujiza na yote yaliyo ndani Yake, na hivyo baadaye Yeye anasema: “Kuna wanyama wa porini wasiohesabika milimani, lakini wote ni wapole kama kondoo mbele Zangu; mafumbo yasiyoeleweka yako chini ya bahari, lakini yanajiwakilisha Kwangu wazi kama vitu vyote vilivyo katika uso wa dunia; katika mbingu juu kuna milki ambayo mwanadamu hawezi kuifikia kamwe, ilhali Natembeatembea katika milki hizo zisizofikika.” Maana ya Mungu ni hii: Ingawa moyo wa mwanadamu ni wa kudanganya kushinda vitu vyote, na huonekana kuwa wa siri yasiyoisha kama jahanamu ya dhana za watu, Mungu hujua hali halisi za watu kama kiganja Chake. Kati ya vitu vyote, mwanadamu ni mnyama mkali na mkatili zaidi kuliko mnyama pori, lakini Mungu amemshinda mwanadamu hadi kiwango ambacho hakuna anayethubutu kuinuka na kupinga. Kwa kweli, kama ilivyo maana ya Mungu, kile watu hufikiria katika mioyo yao ni kigumu kufahamika zaidi kuliko vitu vyote kati ya vitu vyote, hakieleweki, lakini Mungu hauheshimu moyo wa mwanadamu, Anauchukulia tu kama mnyoo mdogo machoni Pake; kwa neno moja kutoka kwa kinywa Chake, Anaushinda, wakati wowote Anapotaka, Anaubwaga, kwa mtikiso kidogo zaidi wa mkono Wake, Anauadibu, na Anauhukumu apendapo.

Leo, watu wote wanaishi katikati ya giza, lakini kwa sababu ya ujaji wa Mungu, watu wanapata kujua kiini cha mwanga kutokana na kumwona Mungu. Katika dunia nzima ni kana kwamba chungu kuu cheusi dunia umepinduliwa juu ya ulimwengu; hakuna awezaye kuvuta pumzi, wote wanataka kugeuza hali, ilhali hakuna ambaye amewahi kukiondoa chungu cheusi.

Ni kwa sababu tu ya kupata mwili kwa Mungu ndipo macho ya watu yamefumbuliwa kwa ghafla, na wamemwona Mungu wa vitendo, na hivyo, Mungu anawauliza kwa sauti ya kuhoji: “Mwanadamu hajawahi kunitambua katika mwanga, lakini ameniona tu katika ulimwengu wa giza. Huko katika hali sawa kabisa na hiyo leo? Ilikuwa katika kilele cha ghasia ya joka kuu jekundu ndipo Nilivaa kirasmi mwili ili kufanya kazi Yangu.” Mungu hafichi kile kinachoendelea katika ufalme wa kiroho, wala Hafichi kile kinachofanyika katika moyo wa mwanadamu, na hivyo tena na tena Yeye huwakumbusha watu: “Siwawezeshi watu Wangu kumjua Mungu mwenye mwili tu, bali pia kuwatakasu. Kwa sababu ya ukali wa amri Zangu za utawala, watu wengi bado wako katika hatari ya kuondolewa na Mimi. Isipokuwa ukifanya juhudi zote kujishughulikia, kuushinda mwili wako mwenyewe, isipokuwa ukifanya hivi, bila shaka utakuwa kitu Ninachodharau na kukataa, cha kutupwa chini kuzimu, jinsi tu Paulo alivyopokea adhabu moja kwa moja kutoka kwa mikono Yangu, ambapo kwayo hakukuwa na kutoroka.” Kadri Mungu anavyosema mambo kama hayo, ndivyo watu wanavyokuwa wenye hadhari na nyayo zao wenyewe zaidi, na ndivyo wanavyoogopa amri za kiutawala za Mungu zaidi, na hapo tu ndipo mamlaka ya Mungu yanaweza kuzalishwa na uadhama Wake kuwekwa wazi. Hapa, Paulo anatajwa mara nyingine ili kuwafanya watu kuelewa mapenzi ya Mungu: Hawapaswi kuwa wale wanaoadibiwa na Mungu, lakini wale wanaozingatia mapenzi ya Mungu. Hili tu ndilo linaloweza kuwafanya watu, katikati ya hofu yao, kukumbuka kutoweza kwa uamuzi wao wa wakati uliopita mbele ya Mungu kumridhisha Mungu kikamilifu, jambo ambalo linawapa majuto makuu hata zaidi, na kuwapa maarifa zaidi ya Mungu wa vitendo, na hivyo hapo tu ndipo wanaweza kuwa bila shaka kuhusu maneno ya Mungu.

“Mwanadamu hanifahamu Mimi tu katika mwili Wangu; zaidi ya haya, ameshindwa kuelewa nafsi yake mwenyewe inayoishi katika mwili. Kwa miaka mingi wanadamu wamekuwa wakinidanganya, wakinichukua kama mgeni kutoka nje. Mara nyingi sana” yanaorodhesha uhalisi wa upinzani wa mwanadamu kwa Mungu, yakionyesha watu mifano ya kweli ya kuadibu; hili ni thibitisho la dhambi, na hakuna awezaye kulikataa tena. Watu wote humtumia Mungu kama chombo cha kila siku, kana kwamba Yeye ni kitu fulani muhimu cha nyumbani ambacho wanaweza kukitumia wapendavyo. Hakuna anayempenda Mungu kwa upendo mkubwa; hakuna ambaye amejaribu kuujua uzuri wa Mungu, wala uso Wake mtukufu, na sembuse yeyote anayekusudia kumtii Mungu. Wala hakuna ambaye amewahi kumtazama Mungu kama kitu kinachopendwa moyoni mwake, wote wanamkokota aje wanapomhitaji, na kumtupa pembeni na kutomjali wasipomhitaji. Ni kana kwamba, kwa mwanadamu, Mungu ni karagosi, ambayo mwanadamu anaweza kuitawala apendapo, na kutoa madai kwa vile apendavyo au atamanivyo. Lakini Mungu anasema, “Kama, katika wakati wa kupata mwili Kwangu, Singekuwa Nimejali kuhusu udhaifu wa mwanadamu, basi binadamu wote, kwa sababu ya kupata mwili Kwangu,

wangetishwa kabisa, na kwa sababu hiyo, wameingia kuzimu,” ambayo inaonyesha tu jinsi umuhimu wa kupata mwili kwa Mungu kulivyo kuuu: Katika mwili, Amekuja kuwashinda wanadamu, badala ya kuwaangamiza wanadamu wote kutoka katika ufalme wa kiroho. Hivyo, Neno lilipokuwa mwili, hakuna aliyejua. Ikiwa Mungu hangekuwa anajali udhaifu wa mwanadamu, ikiwa mbingu na dunia zikageuzwa juu chini Alipopata mwili, watu wote wangekuwa wameangamizwa. Kwa sababu ni desturi ya watu kupenda kilicho kipa na kuchukia kilicho kizee, na mara nyingi wanasahau nyakati mbaya wakati mambo yanaendelea vizuri, na hakuna kati yao ajuaye alivyobarikiwa, hivyo Mungu huwakumbusha tena na tena kwamba wanapaswa kuthamini jinsi leo imepiganiwa kwa nguvu; kwa ajili ya kesho, wanapaswa kuthamini leo hata zaidi, na hawapaswi, kama mnyama, kupanda juu na kutomtambua bwana, na wasikose kujua kuhusu baraka wanazoishi kati yazo. Hivyo, wanakuwa wenye mwenendo mzuri, hawajigambi au kuwa wenye kiburi tena, na wanapata kujua kwamba sio ukweli kwamba asili ya mwanadamu ni nzuri, lakini kwamba huruma na upendo wa Mungu umemjia mwanadamu; wanaogopa kuadibu, na hivyo hawathubutu kufanya zaidi.

Tanbihi:

a. “Mto wa Chu” linarejelea kitamathali mpaka kati ya pande mbili zinazozozana.

Sura ya 13

Mungu anachukia urithi wote wa joka kubwa jekundu, na Hulichukia joka kubwa jekundu hata zaidi. Huu ni mzizi wa ghadhabu iliyo ndani ya moyo wa Mungu. Inaonekana kwamba Mungu anataka kutupa vitu vyote ambavyo ni mali ya joka kubwa jekundu ndani ya ziwa la moto wa jahanamu kuviteketeza kabisa. Kuna nyakati ambazo hata inaonekana kwamba Mungu anataka kuunyosha mkono Wake kuliangamiza binafsi—hilo tu ndilo lingeweza kufuta chuki iliyo ndani ya moyo Wake. Kila mtu katika nyumba ya joka kubwa jekundu ni mnyama anayekosa ubinadamu, ndiyo maana Mungu alizuia kwa nguvu hasira Yake ili kusema yafuatayo: “Miongoni mwa watu Wangu Wote, na miongoni mwa Wanangu wote, yaani, miongoni mwa wale Niliowachagua kutoka kwa wanadamu wote, unapatikana katika kundi la chini zaidi. ...” Mungu ameanza vita vya kuamua mshindi na mshinde dhidi ya joka kubwa jekundu katika nchi yake, na wakati ambapo mpango wake utafaulu Ataliangamiza, Hataliruhusu tena kuwapotosha wanadamu au kuharibu nafsi zao. Hakuna siku ipitayo bila Mungu kuwaita watu Wake ambao wanasinzia ili awaokoe, ilhali wote wameduwaa kana kwamba wamemeza dawa ya usingizi. Asipowaamsha hata kwa dakika moja wanarudi kwa hali yao ya usingizi, bila ufahamu. Inaonekana kwamba watu Wake wote wamepooza kwa thuluthi tatu. Hawajui mahitaji yao wenyewe au kasoro zao wenyewe, au hata wanachopaswa kuvaa au wanachopaswa kula. Inaonyesha kwamba joka kubwa jekundu limetumia kiasi kikubwa cha jitihada kuwapotosha

watu. Ubaya wake unafikia kotekote katika kila mkoa wa Uchina. Hata limewafanya watu kuchukizwa na kutokuwa radhi kuishi tena katika nchi hii ya kuharibika, isiyo na adabu. Kile ambacho Mungu huchukia zaidi ni kiini cha joka kubwa jekundu, ndiyo maana Huwakumbusha watu katika ghadhabu Yake kila siku, na watu huishi chini ya ulinzi wa ghadhabu Yake kila siku. Hata hivyo, wengi sana wa watu bado hawajui kumtafuta Mungu, lakini wao huketi tu wakitazama na kungoja kulishwa kwa mkono. Hata kama wangukuwa wana njaa kabisa hawangukuwa radhi kwenda kutafuta chakula chao wenyewe. Dhamiri za watu zilipotoshwa na Shetani kitambo sana na zikabadilika kwa hali kuwa zisizo na huruma. Si ajabu Mungu alisema: “Kama Mimi Singewazindua, bado usingeamka, lakini, mungeendelea kuwa kama mlioganda, na tena, katika hali ya kubumbwaa.” Ni kana kwamba watu walikuwa kama wanyama ndani ya bumbwaa waliokuwa wakipitisha majira ya baridi na hawakutaka kula au kunywa; hii hasa ni hali ya sasa ya watu wa Mungu, ndiyo maana Mungu huwataka tu watu wamjue Mungu mwenye mwili Mwenyewe katika nuru. Hawashurutishi watu wabadilike kiasi kikubwa au wao kuwa na ukuaji mkubwa katika maisha yao. Hilo lingetoshwa kulishinda joka kubwa jekundu chafu, lenye kutia kinyaa, hivyo kudhihirisha vizuri zaidi nguvu kuu za Mungu.

Watu wanaposoma maneno ya Mungu wanayoweza kufahamu tu ni maana halisi lakini hawawezi kufahamu umuhimu wa kiroho wa maneno hayo. Maneno mawili “mawimbi mabaya” yamemshinda kila shujaa. Ghadhabu ya Mungu inapodhihirishwa, je, maneno Yake, matendo Yake, na tabia Yake si mawimbi yanayopanda na kushuka? Mungu anapowahukumu wanadamu wote, huu si ufichuaji wa ghadhabu Yake? Huu si wakati ambapo mawimbi hayo yanayopanda na kushuka hufanya kazi? Ni nani huyo asiyeishi katikati ya mawimbi yanayopanda na kushuka kwa ajili ya upotovu wa mwanadamu? Yaani, ni nani asiyeishi katikati ya ghadhabu ya Mungu? Wakati ambapo Mungu anataka kugawa msiba mkuu kwa wanadamu, je, kile ambacho watu huona si “dhoruba na mawingu meusi”? Miongoni mwa wanadamu, ni nani asiyeukimbia msiba mkuu? Ghadhabu ya Mungu inamiminika juu ya watu kama mvua nzito na kuwapeperusha kama upepo mkali. Watu wote wanatakaswa kupitia kwa maneno ya Mungu kana kwamba walikuwa wamekumbana na dhoruba ya theluji izungukayo upesi. Ni maneno ya Mungu ambayo hayatambulikani sana kwa wanadamu. Aliuumba ulimwengu kwa kutumia maneno Yake na pia Anawaongoza na kuwatakaswa wanadamu wote kwa kutumia maneno Yake. Na mwisho, Atarudisha tena utakatifu wa ulimwengu wote kwa kutumia maneno Yake. Inaweza kuonekana katika kila sehemu ya maneno Yake kwamba kuweko kwa Roho wa Mungu si uwongo. Watu wanaweza kuona sehemu ya njia ya kuendelea kuishi ndani ya maneno ya Mungu pekee. Watu wote wanaweza kuthamini maneno Yake kwa sababu yana riziki ya maisha. Kadri mwanadamu anavyolenga maneno Yake, ndivyo Atamkabidhi mwanadamu hoja zaidi—hili humfanya kuchanganyikiwa kabisa na akakosa wakati wa kujibu. Maswali ya mfululizo kutoka kwa Mungu

pekee yanatosha kwa watu kutafakari mambo kwa muda fulani, sembuse maneno Yake mengine. Ndani ya Mungu, yote ni kamili na tele na hakuna kinachokosekana. Hata hivyo, watu hawana uwezo wa kufurahia mengi ya hayo; wanajua tu upande wa juujuu wa maneno Yake kana kwamba yote ambayo wangeweza kuona ni ngozi ya kuku lakini hawangeweza kula nyama ya kuku. Hili linamaanisha kwamba watu wana uhaba wa bahati kiasi kwamba hawawezi kumfurahia ndani ya Mungu. Katika fikira za watu kila mmoja wao anashikilia Mungu fulani ndani ya moyo wake, ndiyo maana hakuna anayejua Mungu asiye dhahiri ni nini, au sura ya Shetani ni nini. Kwa hiyo Mungu aliposema “kwa sababu unachokiamini ni sura ya Shetani tu na hakihusiani na Mungu kwa njia yoyote.” watu wote walipigwa bumbuazi kwamba walikuwa wameamini kwa miaka mingi sana, lakini bado hawakuwa wametambua kwamba kile walichokuwa wameamini ni Shetani na si Mungu Mwenyewe. Walihisi uwazi wa ghafula lakini hawakujua la kusema. Wakati huo walianza kuchanganyikiwa tena. Ni kwa kufanya kazi hivi tu ndiyo watu wanaweza kukubali vizuri zaidi nuru mpya na hivyo kukana mambo ya kale. Haijalishi yanavyoonekana kuwa mazuri, hayatakuwa na maana. Ni la manufaa zaidi kwa watu ni kumfahamu Mungu Mwenyewe wa vitendo; hili linawawezesha kujiondolea mioyoni mwao hali ambayo fikira za watu hushikilia humo ndani, na kumruhusu Mungu Mwenyewe awamiliki watu. Ni kwa njia hii tu ndio umuhimu wa kupata mwili unaweza kutimizwa na watu wanaweza kumjua Mungu Mwenyewe wa vitendo kwa macho yao ya mwili.

Mungu amewaambia watu mara nyingi kuhusu hali za ulimwengu wa kiroho. “Shetani anapokuja mbele Yangu, sitetemeki kwa kuuogopa ukali wake, wala kumuogopa kwa sababu ya ubaya wa sura yake: Ninampuuza tu.” Walichoelewa watu kutokana na hili ni hali tu kwa kweli; hawajui ukweli katika ulimwengu wa kiroho. Kwa kuwa Mungu amepata mwili, Shetani ametumia kila aina za mbinu za shutuma, akitaka kumshambulia Mungu kwa njia hii. Hata hivyo, Mungu harudi nyuma kwa sababu ya hili—Anazungumza tu na kufanya kazi miongoni mwa wanadamu na Anawaruhusu watu kumjua kupitia mwili Wake. Shetani amejawa ghadhabu na ametumia kiasi kikubwa cha juhudi kwa watu wa Mungu kuwafanya wawe hasi, warudi nyuma, na hata wapotee njia. Lakini kwa sababu ya athari ya maneno ya Mungu Shetani ameshindwa kabisa, hivyo kuongeza kiwango cha ukali wake. Kwa hivyo, Mungu anamkumbusha kila mtu, “Katika maisha yako, ipo siku itakuja ambayo utakumbana na hali kama hii: Je, utakubali bila kusita kushikwa mateka na Shetani, au utaniruhusu Nikuokoe?” Ingawa watu hawajui mambo yanayotokea katika ulimwengu wa kiroho, punde wasikiapo aina hizi za maneno kutoka kwa Mungu wao hutahadhari na kuogopa—hili hushinda mashambulizi ya Shetani, ambalo linatosha kuonyesha utukufu wa Mungu. Ingawa waliingia katika mbinu mpya ya kufanya kazi zamani sana, watu bado hawana ubayana kuhusu maisha katika ufalme—hata kama wanaelewa, wanakosa ubayana. Kwa hiyo baada ya Mungu kutoa onyo kwa watu,

Aliwasilisha kwao kiini cha maisha katika ufalme: “Maisha katika ufalme ni maisha ya watu na Mungu Mwenyewe.” Kwa vile Mungu Mwenyewe amekuwa mwili, maisha ya mbingu ya tatu yametimizwa hapa duniani. Huu si mpango wa Mungu tu, lakini pia unafanikishwa na Mungu. Muda unapoendelea watu huja kumjua Mungu Mwenyewe zaidi na zaidi na hivyo wanaweza zaidi kuonja maisha yaliyo mbinguni, kwa kuwa wamehisi kweli kwamba Mungu yuko duniani, kwamba Yeye si Mungu asiye dhahiri aliye mbinguni. Kwa hiyo, maisha duniani ni sawa na yale yaliyo mbinguni. Ukweli ni kwamba Mungu anakuwa mwili na Anaonja uchungu wa ulimwengu wa binadamu, na kadri Anavyoweza kuonja uchungu huo katika mwili, ndivyo inavyothibitisha zaidi kwamba Yeye ni Mungu Mwenyewe wa vitendo. Hii ndiyo maana maneno yafuatayo yanatosha kuthibitisha utendaji wa Mungu wa leo: “Katika makao Yangu, ambayo ni sehemu Nilipojificha, hata hivyo, katika haya makao Yangu, Nimewashinda maadui Wangu wote; katika makao Yangu, Nimepata uzoefu wa kuishi duniani; katika makao Yangu, Ninalichunguza kila neno na tendo la mwanadamu, na kuchungulia na kuongoza wanadamu wote.” Kuishi katika mwili kwa kweli, kupitia maisha ya mwanadamu katika mwili kwa kweli, kufahamu binadamu wote kutoka ndani ya mwili kwa kweli, kuwashinda wanadamu katika mwili kwa kweli, kupigana vita vya kuamua mshindi na mshinde na joka kubwa jekundu katika mwili kwa kweli, na kufanya kazi yote ya Mungu katika mwili—je, huku hasa si kuweko kwa Mungu Mwenyewe wa vitendo? Ihali, ni nadra sana kuwapata watu wanaoweza kuona ustadi katika maneno haya ya kawaida yaliyonenwa na Mungu. Wao huyapitiapitia tu, na hawahisi thamani au uadimifu wa maneno ya Mungu.

Maneno ya Mungu hugeuka vizuri sana—msemu “Mwanadamu akiwa kwenye usingizi mzito” unageuza ufafanuzi wa Mungu Mwenyewe kuwa ufafanuzi wa hali ya wanadamu wote. Hapa, “milipuko ya mwanga baridi” hayawakilishi umeme wa Mashariki, lakini ni maneno ya Mungu, yaani, mbinu Yake mpya ya kufanya kazi. Hivyo, katika hili aina zote za nguvu za watu zinaweza kuonekana: Baada ya kuingia katika mbinu mpya, wote wanapoteza mwelekeo wao, wasijue wanakotoka wala wanakoenda. “Watu wengi hufumwa na mwanga huu” yanahusu watu waliotolewa kupitia mbinu mpya, wale wasioweza kuhimili majaribio au kustahamili usafishaji wa mateso na hivyo wanatupwa kuzimu mara nyingine. Neno la Mungu huwafichua wanadamu kwa kiwango fulani—inaonekana kwamba watu huogopa wanapoyaona maneno ya Mungu, na hawathubutu kusema lolote kana kwamba tu wameona mtutu wa bunduki umeelekezwa moja kwa moja kwa mioyo yao. Hata hivyo, wao pia wanahisi kwamba kuna mambo mazuri katika maneno ya Mungu. Mioyo yao imezozana sana na hawajui wanachopaswa kufanya, lakini kwa sababu ya imani yao, yote wafanyayo ni kujizatiti na kutafuta zaidi katika maneno Yake wakihofu kwamba Mungu atawaacha. Kama tu alivyosema Mungu: “ni nani miongoni mwa wanadamu hayumo katika hali sawa na hii? Ni nani hayumo katika mwangaza Wangu? Hata

kama wewe ni mwenye nguvu, au hata kama wewe ni mnyonge, ni vipi waweza kuepuka ujio wa mwanga Wangu?” Mungu akimtumia mtu, hata kama ni mnyonge, Mungu bado Atamwangaza na kumpa nuru katika kuadibu Kwake, kwa hivyo kadri watu wanavyosoma maneno ya Mungu, ndivyo wanavyomfahamu zaidi, ndivyo wanavyomcha zaidi, na ndivyo wanavyopunguza kuthubutu kuwa wazembe. Kwamba watu wamefika hapa leo ni kwa sababu tu ya nguvu kuu za Mungu. Ni kwa sababu ya mamlaka ya maneno Yake, yaani, ni kwa ajili ya Roho aliye ndani ya maneno Yake ndiyo watu wanamcha Mungu. Kadri Mungu anavyofichua sura halisi ya wanadamu, ndivyo wanavyomheshimu zaidi, hivyo ndivyo wanavyokuwa na hakika zaidi kuhusu uhalisi wa kuwepo Kwake. Huu ni mnara wa Mungu ulio njiani kwa wanadamu kumfahamu Mungu; huu ni ujia ambao Mungu amewapa kuufuata. Mkifirikia kwa makini kulihusu, je sivyo?

Je, yaliyosemekana hapo juu si mnara ulio njiani mbele ya wanadamu?

Sura ya 14

Mwanadamu hajawahi kamwe kujifunza chochote kutoka kwa neno la Mungu. Badala yake, mwanadamu huthamini tu umbo la nje la neno la Mungu, lakini kutojua maana yake halisi. Kwa hivyo, ingawa wengi wa watu wanapenda neno la Mungu, Mungu asema kwamba hawalithamini kwa kweli. Hili ni kwa sababu katika maoni ya Mungu, hata ingawa neno Lake ni kitu cha thamani, watu hawajaonja utamu wake halisi. Kwa hivyo, wanaweza tu “kukata kiu chao na mawazo ya matunda kama zambarau,” na hivyo kutuliza mioyo yao yenye tamaa. Roho wa Mungu hafanyi tu kazi miongoni mwa watu wote, pia kuna kupata nuru kwa neno la Mungu. Ni vile tu watu hawajali sana kiasi kwamba hawawezi kuthamini kweli kiini chake. Katika akili ya mwanadamu, sasa ndiyo enzi ya ufalme inatambuliwa kabisa, lakini kwa kweli huu si ukweli. Ingawa kile ambacho Mungu hutabiri ni kile ambacho Amefanikisha, ufalme halisi bado haujasili duniani kabisa. Badala yake, pamoja na mabadiliko katika wanadamu, pamoja na maendeleo katika kazi, na pamoja na umeme unaotoka Mashariki, yaani, pamoja na kuzidi kwa neno la Mungu, ufalme utajitokeza polepole duniani, utakuja duniani polepole lakini kwa ukamilifu. Mchakato wa kuwasili kwa ufalme pia ni mchakato wa kazi takatifu duniani. Wakati huo huo, kote kote ulimwenguni, Mungu ameanza kazi ambayo haijafanywa katika enzi zote katika historia nzima: Kuupanga ulimwengu mzima upya. Kwa mfano, mabadiliko makubwa mno yanaonekana kote kote ulimwenguni, ikiwa ni pamoja na mabadiliko katika Taifa la Israeli, mapinduzi ya serikali Marekani, mabadiliko katika Misri, mabadiliko katika Mwingano wa Baraza la Kirusi, na kuangushwa kwa Uchina. Wakati ambapo ulimwengu wote utakuwa umetulia na utakuwa umerudishwa kuwa kawaida, huo ndio wakati ambapo kazi ya Mungu duniani itakamilishwa; huo ndio wakati ambapo ufalme utakuja duniani. Hii ni maana ya kweli

ya maneno “Wakati mataifa yote ya dunia yata vurugwa, hapo ndipo hasa ufalme Wangu utanzishwa na kupata umbo na pia Nitabadilika na kurejea kwa ulimwengu mzima.” Mungu hawafichi wanadamu chochote, Amewaambia watu siku zote kuhusu utajiri Wake wote, lakini hawawezi kuelewa maana Yake, wao hukubali tu neno Lake kama wapumbavu. Katika hatua hii ya kazi, wanadamu wamejifunza kutoeleweka kwa Mungu, na zaidi ya hayo, wanaweza kutambua vyema ugumu wa kazi ya kumfahamu; kwa sababu hii, wamehisi kwamba siku hizi, kumwamini Mungu ni jambo gumu zaidi kufanya, sawa na kumfundisha nguruwe kuimba. Hawana uwezo kabisa kama panya aliyekwama ndani ya mtego. Kwa kweli, haijalishi mtu ana nguvu kiasi gani au jinsi ujuzi wa mtu ulivyo stadi, au kama mtu ana uwezo usio na kikomo ndani yake, inapohusu neno la Mungu mambo haya hayana maana yoyote. Ni kana kwamba wanadamu ni rundo la jivu la karatasi lililotekelea machoni pa Mungu, bila thamani yoyote kabisa, sembuse matumizi yoyote. Hiki ni kielezo kamili cha maana ya kweli ya maneno “Nimekuwa, kwa maoni yao, Nimefichwa zaidi na zaidi kutoka kwake na Nikazidi kutoeleweka na wao.” Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba kazi ya Mungu hufuata uendeleaji wa kawaida na hutekelezwa kutegemea kile ambacho ogani za wanadamu za utambuzi zinaweza kuelewa. Wakati ambapo asili ya wanadamu ni imara na thabiti, maneno anenayo Mungu hupatana kabisa na dhana zao na huonekana kana kwamba dhana za Mungu na za wanadamu ni kitu kimoja, bila tofauti yoyote kabisa. Hili huwafanya watu waujue uhalisi wa Mungu kwa kiasi fulani, lakini hili silo lengo kuu la Mungu. Mungu anawaruhusu watu kutulia kabla ya kuanza rasmi kazi Yake ya kweli duniani. Kwa hivyo, wakati wa mwanzo huu ambao ni wa kuwatatanisha wanadamu, wanadamu wanatambua kwamba mawazo yao ya awali hayakuwa sahihi na kwamba Mungu na mwanadamu wanatofautiana kama mbingu na dunia na hawafanani kabisa. Kwa sababu maneno ya Mungu hayawezi tena kutathminiwa kutegemea dhana za wanadamu, mwanadamu mara moja anaanza kumfahamu Mungu vinginevyo, na kwa sababu hii anaanza kumkazia Mungu macho kwa mshangao, kana kwamba Mungu wa vitendo ni mkali kama Mungu asiyeonekana na Asiyegusika, kana kwamba mwili wa Mungu uko nje pekee na hauna kiini Chake. Licha ya ukweli kwamba Roho wa Mungu amepata mwili, Anaweza kujigeuza kuwa umbo la Roho na kutoweka kwa kuelea wakati wowote; watu wamekuza mtazamo wa hadhari kwa kiasi fulani. Mungu anapotajwa, watu humvisha mavazi na dhana zao, wakisema Anaweza kupanda juu ya mawingu na ukungu, Anaweza kutembea juu ya maji, Anaweza kuonekana na kutoweka ghafla miongoni mwa wanadamu, na wengine hata wana fafanuzi zaidi za kutoa wasifu. Kwa sababu ya kutojua kwa wanadamu na kukosa umaizi, Mungu alisema “wakati wameamini wamenipinga ama kukosea amri Zangu za kitawala, Nafunga macho.”

Wakati ambapo Mungu hufichua upande mbaya na ulimwengu wa ndani wa wanadamu,

Yeye daima huwa sahihi kabisa, bila mkengeuko hata kidogo. Hata inaweza kusemwa kwamba hakuna kosa kwa vyovyote vile. Hili ni thibitisho linalowaridhisha watu kabisa. Kwa sababu ya kanuni ya kazi ya Mungu, mengi ya maneno Yake na matendo huacha alama ambayo haiwezi kufutwa, na watu huonekana kuwa na hata ufahamu mkubwa zaidi kumhusu Yeye, kana kwamba wanagundua mambo ambayo ni ya thamani zaidi ndani Yake. “Kwa kumbukumbu zao, mimi ni Mungu anayeonyesha huruma kwa wanadamu badala ya kuwarudi, ama Mimi ni Mungu Mwenyewe asiyemaanisha Anachokisema. Haya yote ni mawazo yanayotokana na fikira za wanadamu na sio kwa mujibu na ukweli.” Ingawa wanadamu hawajawahi kamwe kutilia maanani uso halisi wa Mungu, wanajua “upande wa kando wa tabia Yake” vizuri sana; wao daima hutafuta makosa katika maneno na matendo ya Mungu. Hili ni kwa sababu wanadamu huwa radhi kila mara kuzingatia vitu hasi, na kupuuza vitu vya hakika, wakidunisha tu matendo ya Mungu. Kadri Mungu anavyosema kwamba Yeye hujificha kwa unyenyekevu katika makao Yake, ndivyo binadamu wanavyomwekea Yeye madai mengi zaidi. Wanasema, “Ikiwa Mungu mwenye mwili anatazama kila kitendo cha binadamu na kupitia maisha ya binadamu, kwa nini kwamba wakati mwingi Mungu hajui kuhusu hali zetu halisi? Je, lina maana kwamba Mungu amejificha kweli?” Ingawa Mungu hutazama ndani kabisa ya moyo wa mwanadamu, Yeye bado hufanya kazi kufuatana na hali halisi za wanadamu, bila kuwa asiye yakini wala wa mwujiza. Ili kuondoa kabisa tabia ya zamani ndani ya wanadamu, Mungu ametumia kila juhudi kunena kutokana na mitazamo mbalimbali: Akifunua asili yao halisi, Akitamka hukumu kwa uasi wao; wakati mmoja Akisema Atashughulikia watu wote, na wakati mwingine Akisema Ataokoa kundi la watu; ama Akiwapa wanadamu masharti au Anawaonya; kwa zamu Akichangua sehemu yao ya ndani, kwa zamu Akitoa matibabu. Hivyo, chini ya uongozi wa neno la Mungu, ni kana kwamba wanadamu walikuwa wamesafiri kwenda kwa kila pembe ya dunia na wakaingia katika bustani karimu ambapo kila ua linashindana kuwa zuri kupita yote. Chochote asemacho Mungu wanadamu wataingia katika neno Lake, kana kwamba Mungu ni sumaku na chochote chenye chuma kitavutiwa kwake. Wanapooni maneno “Binadamu hawanitambui, hivyo nami pia Siutilii maanani. Wanadamu hawanitambui, kwa hivyo Mimi pia Siweki juhudi kwao. Je, hii ni bora?” inaonekana watu wote wa Mungu wameangushwa kuzimu tena, au kugongwa tena katika sehemu zao za uhai, wakiwachwa wameshtuka kabisa. Hivyo, wao wanaingia tena katika mbinu. Wanatatanihwa hasa kuhusiana na maneno “Iwapo, kama mmoja wa watu Wangu kwenye ufalme, huwezi kufanya wajibu wako, utachukiwa na kukataliwa na Mimi!” Watu wengi sana wamesababishwa kuwa na machozi ya kuhuzunisha sana: “Nilikuwa na wakati mgumu kujiondoa kuzimu, kwa hiyo Singekuwa na tumaini kabisa ikiwa Ningeanguka ndani yake tena. Sijapata chochote katika ulimwengu wa wanadamu, nikipitia kila aina ya taabu na matatizo katika maisha yangu. Hasa, baada ya kuingia katika imani, nilipitia hali ya kuachwa na wapendwa, mateso kutoka kwa familia, kashfa kutoka kwa watu wa dunia, na sikufurahia raha

ya ulimwengu. Nikianguka tena kuzimu, maisha yangu hayatakuwa bure hata zaidi?” (Kadri mwanadamu anavyofikiria kuhusu hili ndivyo anavyohisi huzuni zaidi.) “Matumaini yangu yote yamekabidhiwa mikononi mwa Mungu. Mungu akiniacha, heri nife sasa.... Kwa hakika, yote yamejaaliwa na Mungu, sasa naweza tu kutaka kumpenda Mungu, mengine yote ni ya baadaye. Ni nani alifanya hili kuwa majaaliwa yangu?” Kadri mwanadamu anavyofikiria, ndivyo anavyokuwa karibu zaidi na viwango vya Mungu na kusudi la maneno Yake. Kwa njia hii lengo la maneno Yake linatimizwa. Baada ya wanadamu kuyaona maneno ya Mungu wote huwa na mapambano ya itikadi ndani yao. Chaguo lao pekee ni kutii masharti ya majaaliwa, na kwa njia hii lengo la Mungu hutimizwa. Kadri maneno ya Mungu yalivyo makali, ndivyo ulimwengu wa ndani wa wanadamu unavyokuwa mgumu zaidi kufahamika kutokana na hilo. Huku ni kama kugusa kidonda; kadri kinavyoguswa kwa nguvu ndivyo kinavyouma zaidi, kiasi kwamba wanakaribia kifo na hata kukata tamaa ya kuendelea kuishi. Kwa njia hii, wakati ambapo wanadamu huteseka zaidi tu na wakiwa wamezama katika kutaka tamaa ndipo wanaweza kutoa mioyo yao halisi kwa Mungu. Asili ya wanadamu ni kwamba hata chembe ya tumaini ikibaki hawatamwendea Mungu kupata msaada, lakini watachukua mbinu za kujitosheleza za kuendelea kudumu kwa kawaida. Hili ni kwa sababu asili ya wanadamu ni ya kujidai, na wao humdharau kila mtu. Kwa hivyo, Mungu alisema: “hakuna mwanadamu hata mmoja ameweza kunipenda pia akiwa na faraja. Hakuna mtu hata mmoja amenitafuta wakati wa amani na furaha ili Nishiriki furaha yake.” Hili kweli ni la kusikitisha: Mungu aliwaumba wanadamu, lakini Anapokuja kwa ulimwengu wa wanadamu, watu hutaka kumpinga na humfukuza kutoka kwa eneo lao, kana kwamba Yeye ni yatima fulani tu, akielea duniani, au kama mtu wa dunia asiye na nchi. Hakuna mtu anayehisi kumpenda Mungu sana, hakuna mtu anayempenda kweli, hakuna mtu ambaye amekaribisha kuja kwake. Badala Yake, wanapooni kuja kwa Mungu, kufumba na kufumbua nyuso zao za furaha huwa na huzuni, kana kwamba dhoruba ya ghafula inakaribia, kana kwamba Mungu angeondoa raha ya familia zao, kana kwamba Mungu hakuwahi kamwe kuwabariki wanadamu, lakini badala yake Alikuwa Amewapa wanadamu taabu. Kwa hivyo, katika akili za wanadamu, Mungu si mwandani kwao, lakini Yule ambaye daima huwalaani; kwa hivyo, wanadamu hawamtilii maanani, hawamkaribishi, kila mara wao huwa hasimu Kwake, na hili halijawahi kubadilika kamwe. Kwa sababu wanadamu wana mambo haya katika mioyo yao, Mungu asema wanadamu hawana akili na ni waovu, na kwamba hata hisia ambazo wanadamu kwa kuwazia wamejizatiti nazo haziwezi kuonekana ndani yao. Wanadamu hawadhihirishi fikira yoyote kwa hisia za Mungu, lakini hutumia kinachoitwa “haki” kumshughulikia Mungu. Wanadamu wamekuwa hivi kwa miaka mingi na kwa sababu hii Mungu amesema tabia yao haijabadilika. Hili linaonyesha wazi kwamba hawana dutu linalozidi manyoya machache. Inaweza kusemwa kwamba wanadamu ni wanyonge wasio na thamani kwa sababu hawajithamini. Kama hata hawajipendi, bali hujikandamiza, hili halionyeshi kwamba hawana

thamani? Wanadamu ni kama mwanamke mwovu ambaye hujihadaa na ambaye hujitoa kwa wengine kwa hiari kuingiliwa bila heshima. Lakini hata hivyo, bado hawajui vile walivyo duni. Wao hufurahia kuwatumikia wengine, au kuzungumza na wengine, kujiweka chini ya utawala wa wengine; huu kweli si uchafu wa wanadamu? Ingawa Sijapitia maisha miongoni mwa wanadamu, kwa vile Sijapitia kweli maisha ya binadamu, Nina ufahamu kamili wa kila mwendo, kila hatua, kila neno, na kila kitendo cha mwanadamu. Naweza hata kuwaweka wanadamu wazi mpaka waaibike kabisa, kiasi cha kutoweza tena kuthubutu kuonyesha hila zao na kutoweza tena kuthubutu kujiachilia kwa tamaa zao. Kama konokono ambaye hurudi ndani ya kombe lake, hawathubutu tena kuonyesha hali zao mbaya. Kwa sababu wanadamu hawajijui, dosari yao kubwa sana ni kuonyesha kwa hiari haiba yao mbele ya wengine, wakionyesha sura yao mbaya; Hiki ni kitu ambacho Mungu hukichukia zaidi. Kwa sababu mahusiano kati ya watu si ya kawaida, na hakuna mahusiano ya kawaida ya mtu mmoja na mwingine kati ya watu, sembuse uhusiano wa kawaida kati yao na Mungu. Mungu amesema mengi sana, na kwa kufanya hivyo lengo Lake kuu ni kumiliki nafasi ndani ya mioyo ya wanadamu, kuwafanya watu waondoe sanamu zote ndani ya mioyo yao, ili Mungu aweze kuwatawala wanadamu wote na Atimize lengo Lake la kuwa duniani.

Sura ya 15

Tofauti kubwa kabisa kati ya Mungu na mwanadamu ni kwamba maneno ya Mungu hulenga kiini cha jambo moja kwa moja, bila kuficha chochote. Hivyo, kipengele hiki cha tabia ya Mungu kinaweza kuonekana katika sentensi ya kwanza ya leo. Inafunua hali halisi za mwanadamu mara moja na kufichua tabia ya Mungu. Ni chanzo cha vipengele kadhaa vya uwezo wa maneno ya Mungu kufanikisha matokeo. Hata hivyo, watu hushindwa kufahamu hili; kila wakati wao huja kujijua kupitia katika maneno ya Mungu, bila ya “kumchambua” Mungu. Ni kana kwamba wanaogopa kumkosea Yeye au kwamba Atawaua kwa sababu ya “uangalifu” wao. Kwa kweli, watu wengi wanapokula na kunywa neno la Mungu, hufanya hivyo kutoka katika mtazamo hasi, sio ulio chanya. Inaweza kusemwa kuwa watu sasa wameanza “kuzingatia unyenyekevu na utiifu” chini ya mwongozo wa maneno Yake. Kutokana na hili, ni dhahiri kwamba watu wameanza kuzidi mipaka kwa namna nyingine—kutoka kwa kutokuwa makini na maneno Yake kuelekea kuyapa uzingativu usiostahili. Hata hivyo, hakuna mtu hata mmoja ambaye ameingia kutoka katika mtazamo chanya, wala hakuna mtu yeyote aliyewahi kujua kweli lengo la Mungu la kuwafanya wanadamu wazingatie maneno Yake. Inajulikana kutoka katika yale ambayo Mungu anasema kwamba Yeye hahitaji kupitia maisha ya kanisa binafsi ili kuweza kuelewa, kwa usahihi na bila makosa, hali halisi za watu wote waliyomo. Kwa sababu wamepata kuingia tu katika njia mpya, watu bado hawajaweza kuondokana kabisa na vipengele hasi; harufu za maiti bado zinaenea katika kanisa lote. Ni kana kwamba watu wamemeza dawa

hivi punde na bado wametunduwazwa, ufahamu wao bado haujarejeshwa kikamilifu. Ni kana kwamba bado wanatishiwa na kifo, ili kwamba, wakiwa katikati ya hofu, hawawezi kuvuka mipaka wenyewe. “Wanadamu wote ni viumbe wasio na ufahamu kujihusu”: Namna ambavyo kauli hii inasemwa bado ina msingi katika ujenzi wa kanisa. Licha ya ukweli kwamba watu wote kanisani huzingatia maneno ya Mungu, asili zao zimekita mizizi kwa njia isiyochangulika. Hii ndiyo maana Mungu alizungumza jinsi alivyozungumza katika hatua iliyopita kuwahukumu watu, ili wapate kukubali kupigwa na maneno Yake katikati ya kiburi chao. Ingawa watu walipitia miezi mitano ya usafishaji kwenye shimo lisilo na mwisho, hali yao halisi bado ni ile ya kutomjua Mungu. Bado ni waovu; wanakuwa tu waliojilinda dhidi ya Mungu. Hatua hii ndiyo hatua ya kwanza inayofaa ambayo watu huchukua katika njia ya kuyajua maneno ya Mungu; hivyo, katika kuunganishwa na kiini cha maneno ya Mungu, si vigumu kuona kwamba sehemu ya hapo awali ya kazi iliandaa njia kwa ajili ya leo, na kwamba ni sasa tu ndiyo kila kitu kimefanywa kuwa kawaida. Udhaifu mbaya wa watu ni tabia yao ya kutenganisha Roho wa Mungu na nafsi Yake ya mwili ili kupata uhuru wa kibinafsi na kuepuka kizuizi cha kila wakati. Hii ndiyo sababu Mungu huwafafanua wanadamu kama ndege wadogo “wakirukaruka huku na kule kwa furaha.” Hii ndiyo hali halisi ya wanadamu wote. Hiyo ndiyo huwafanya watu wote wawe rahisi kuwashinda, na ndipo mahali ambapo wana uwezekano mkubwa zaidi wa kupoteza njia yao. Ni dhahiri katika hili kwamba kazi ya Shetani kati ya wanadamu si zaidi ya kazi hii. Kadiri inavyofanywa zaidi na Shetani ndani ya watu, ndivyo mahitaji ya Mungu kwao yanavyozidi kuwa makali zaidi. Anawahitaji watu waweke mawazo yao katika maneno Yake, ilhali Shetani anafanya kazi kwa bidii kuivunja. Hata hivyo, Mungu daima huwakumbusha watu wazingatie zaidi maneno Yake; hiki ndicho kilele cha vita vinavyotanda katika ulimwengu wa kiroho. Inaweza kusemwa kwa njia hii: Kile ambacho Mungu anataka kufanya ndani ya mwanadamu ndicho ambacho Shetani anataka kuharibu hasa, na kile ambacho Shetani anataka kuharibu kinaonyeshwa kupitia katika mwanadamu, bila kufichwa hata kidogo. Kuna mifano ya wazi ya kile ambacho Mungu hufanya ndani ya watu: Hali zao zinaendelea kuwa bora zaidi na zaidi. Pia kuna maonyesho ya wazi ya uharibifu wa Shetani ndani ya wanadamu: Wanazidi kuwa wapotovu, na hali zao zinazidi kuzorota. Punde hali zinapokuwa duni kabisa, wanakuwa na uwezekano wa kutekwa na Shetani. Hii ndiyo hali halisi ya kanisa, kama ilivyoonyeshwa katika maneno ya Mungu, na pia ndiyo hali halisi ya ulimwengu wa kiroho. Ni onyesho la elimumwendo za ulimwengu wa kiroho. Ikiwa watu hawana imani ya kushirikiana na Mungu, basi wamo katika hatari ya kutekwa na Shetani. Huu ni ukweli. Ikiwa mtu anaweza kweli kuutoa moyo wake kikamilifu ili Mungu aumiliki, basi hivyo ni kama vile Mungu alivyosema: “... ambaye, wakati ako mbele Yangu, anaonekana kuwa katika kumbatio Langu, akionja joto lake.” Hili linaonyesha kuwa mahitaji ya Mungu kwa wanadamu si ya juu; Anawahitaji tu wainuke na kushirikiana na Yeye. Je, hili si jambo rahisi na la furaha? Je, hiki ndicho kitu kimoja ambacho

kimemfadhaisha kila shujaa na mtu mkubwa? Ni kama kwamba majemadari walikuwa wamechukuliwa kutoka kwenye uwanja wa vita na walazimishwe kushona badala yake—“mashujaa” hawa wamelemazwa na ugumu, na hawajui la kufanya.

Kipengele chochote cha mahitaji ya Mungu kwa wanadamu kilicho kikubwa zaidi, hicho ndicho kipengele ambacho kwacho mashambulio ya Shetani kwa binadamu yatakuwa makali zaidi, na hivyo, hali za watu wote zinafunuliwa ipasavyo. “Ni yupi kati yenu mliosimama mbele Yangu atakuwa safi kama theluji na asiye na lawama kama jiwe la thamani?” Watu wote bado wanamrairai Mungu na kuficha vitu kutoka Kwake; bado wanatekeleza njama zao maalum. Hawajaweka mioyo yao kabisa mikononi mwa Mungu ili kumridhisha, lakini wanatamani kupata thawabu Zake kwa kuwa wenye shauku. Watu wanapokula chakula kitamu, wanamweka Mungu kando, wakimwacha Akisimama pale, akisubiri “kushughulikiwa”; watu wanapokuwa na mavazi mazuri, wao husimama hapo mbele ya kioo, wakifurahia uzuri wao wenyewe, na ndani ya mioyo yao, hawamridhishi Mungu. Wanapokuwa na hadhi, wanapokuwa na starehe za anasa, wao hukaa hapo juu ya hadhi zao na kuanza kufurahia, lakini hawajinyenyekezi kwa sababu ya kuinuliwa na Mungu. Badala yake, wao husimama katika maeneo yao ya juu, wakiongea maneno yao ya kifahari, na hawazingatii uwepo wa Mungu, wala hawatafuti kujua thamani Yake. Watu wanapokuwa na mungu mioyoni mwao, au mioyo yao inapokuwa imechukuliwa na mtu mwingine, inamaanisha kuwa tayari wamekataa uwepo wa Mungu, kana kwamba Yeye ni mdukizi mioyoni mwao. Wanaogopa kwamba Mungu ataiba upendo wa wengine kwao na kwamba baadaye watahisi upweke. Kusudi la asili la Mungu ni kwamba hakuna kitu duniani kinapaswa kuwafanya watu wampuuze, na ingawa kunaweza kuwa na upendo kati ya watu, bado Mungu hawezi kufukuzwa kutoka katika “upendo” huu. Vitu vyote vya kidunia ni tupu—hata hisia kati ya watu ambazo haziwezi kuonekana au kuguswa. Bila uwepo wa Mungu, viumbe vyote vitarudi kuwa bure. Duniani, watu wote wana vitu ambavyo wanapenda, lakini hakuna mtu ambaye amewahi kuyachukua maneno ya Mungu kama kitu anachopenda. Hii inaamua kiwango ambacho watu wanayaelewa maneno Yake. Ingawa maneno Yake ni makali, hakuna mtu anayejeruhiwa nayo, kwa maana watu hawayatili maanani kwa kweli; badala yake, wanayachunguza kama wanavyolichunguza ua. Hawachukulii maneno Yake kama matunda ili waweze kuyaonja wenyewe, kwa hivyo hawajui kiini cha maneno ya Mungu. “Kama wanadamu wangependa kweli kuona ukali wa upanga Wangu, wangepimbia kwa hofu hadi ndani ya mashimo kama panya.” Mtu aliye katika hali ya mtu wa kawaida, baada ya kusoma maneno ya Mungu, atakuwa mwenye kushangaa, aliyejaa aibu na asiyeweza kuonana na wengine. Hata hivyo, siku hizi, watu ni kinyume kabisa—wao huyatumia maneno ya Mungu kama silaha kuwapiga wengine. Kwa kweli hawana aibu!

Matamko ya Mungu yametuleta katika hali hii ya kuwepo: “Ndani ya ufalme, si tu kwamba

matamko hutoka kinywani Mwangu, lakini miguu Yangu inatembea kwa heshima kila mahali katika nchi zote.” Katika vita kati ya Mungu na Shetani, Mungu anashinda kila hatua ya njia. Anapanua kazi Yake kwa kiwango kikubwa katika ulimwengu wote, na inaweza kusemwa kwamba kila mahali kuna nyayo za miguu Yake na ishara za ushindi Wake. Katika njama zake, Shetani anatumaini kuharibu usimamizi wa Mungu kwa kuzigawanya nchi, lakini Mungu amechukua fursa ya kusalimu amri huku kupanga upya ulimwengu mzima—ingawa si ili kuuangamiza wote. Mungu hufanya kitu kipya kila siku, lakini watu hawajatambua. Hawazingatii elimumwendo za ulimwengu wa kiroho, kwa hivyo hawawezi kuiona kazi mpya ya Mungu. “Ndani ya ulimwengu, kila kitu huangaza kama kipya katika mwangaza wa utukufu Wangu, kikitoa kipengele chenye kufurahisha ambacho hufurahisha akili na kuinua roho za watu, kana kwamba uko katika mbinguni iliyo zaidi ya mbingu, kama inavyodhaniwa katika fikira za binadamu, ambazo hazijanajisiwa na Shetani na zisizo na mashambulizi ya maadui wa nje.” Hii inatabiri tukio la kufurahisha la ufalme wa Kristo duniani, na pia inajulisha hali ya mbingu ya tatu kwa wanadamu: Ni vitu hivyo vitakatifu pekee ambavyo ni vya Mungu ndivyo vipo huko, bila mashambulizi yoyote ya nguvu za Shetani. Lakini kilicho muhimu zaidi ni kuwaruhusu watu kuona hali za kazi hapa duniani kwa Mungu Mwenyewe: Mbingu ni mbingu mpya, na kuifuata, vivyo hivyo dunia inafanywa upya. Kwa sababu haya ni maisha chini ya mwongozo wa Mungu, watu wote wana furaha isiyo na kipimo. Katika ufahamu wao, Shetani ni “mfungwa” wa wanadamu, na hawaogopi au huogopa kwa sababu ya uwepo wake. Kwa sababu ya maagizo ya moja kwa moja na mwongozo kutoka kwa Mungu, njama zote za Shetani zimekuwa bure, na hili hata linatosha kuthibitisha kwamba Shetani hayupo tena, kwa kuwa ameangamizwa na kazi ya Mungu. Hiyo ndiyo maana inasemekana, “... uko katika mbinguni iliyo zaidi ya mbingu.” Mungu aliposema, “Hakuna usumbufu umewahi kutokea, wala ulimwengu haujawahi kugawanyika,” Alikuwa akimaanisha hali ya ulimwengu wa kiroho. Hili ni thibitisho kwamba Mungu anatangaza ushindi juu ya Shetani, na ni ishara ya ushindi wa mwisho wa Mungu. Hakuna mwanadamu anayeweza kubadilisha mawazo ya Mungu, wala hakuna anayeweza kuyajua. Ingawa watu wamesoma maneno ya Mungu na kuyachunguza kwa uzito, bado wanashindwa kuonyesha kiini chake. Kwa mfano, Mungu alisema, “Ninaruka kwa kupaa juu ya nyota, na jua linapotoa miali yake, Ninalizuia joto la miali hiyo, Nikituma chembe kubwa za theluji kiwango cha manyoya ya bata bukini yakielea kwenda chini kutoka katika mikono Yangu. Hata hivyo, Ninapobadili mawazo Yangu, theluji yote inayeyuka na kuwa mto, na papo hapo, majira ya kuchipua yameibuka kila mahali chini ya anga na zamaradi ya kijani imeyageuza mazingira yote juu ya dunia.” Ingawa watu wanaweza kufikiria maneno haya katika akili zao, kusudi la Mungu si rahisi sana. Wakati kila mtu aliye chini ya mbingu amepigwa na bumbuwazi, Mungu hutamka sauti ya wokovu, na hivyo kuiamsha mioyo ya watu. Hata hivyo, kwa sababu misiba ya kila aina inawapata, wanahisi hali ya ukiwa ya ulimwengu, kwa hivyo

wote wanatafuta kifo na wanaishi katika mapango baridi yenye barafu. Wanagandizwa na baridi ya dhoruba kubwa ya theluji, kiasi kwamba hawawezi kuishi kwa sababu ya ukosefu wa joto duniani. Ni kwa sababu ya upotovu wa watu ndiyo wanauana kwa ukatili zaidi na zaidi. Na kanisani, watu wengi watamezwa kwa mmezo mmoja na joka kubwa jekundu. Baada ya majaribu yote kupita, usumbufu wa Shetani utaondolewa. Ulimwengu mzima, katikati ya mabadiliko, hivyo utapenyezwa na msimu wa kuchipua, joto litaifunika dunia, na dunia itajaa nguvu. Hizi zote ni hatua za mpango mzima wa usimamizi. “Usiku” ambao Mungu alizumngumzia unarejelea wakati ambapo wazimu wa Shetani atafika kilele chake, tukio ambalo litatokea usiku. Je, hilo silo linalofanyika hivi sasa? Ingawa watu wote huishi chini ya mwongozo wa nuru ya Mungu, wanapitishwa katika taabu za giza la usiku. Ikiwa hawawezi kuepuka pingu za Shetani, wataishi milele katikati ya usiku wenye giza. Tazama nchi za dunia: Kwa sababu ya hatua za kazi ya Mungu, nchi za dunia “zinakimbia huku na kule,” na kila moja “inatafuta hatima yake inayofaa.” Kwa sababu siku ya Mungu bado haijafika, kila kitu duniani kinabaki katika mchafuko wa matope. Wakati atakapoonekana wazi kwa ulimwengu wote, utukufu Wake utaujaza Mlima Sayuni, na vitu vyote vitakuwa taratibu na safi, kwa kuwa vitapangwa na mikono Yake. Maneno ya Mungu hayazungumzi kuhusu leo tu, lakini pia yanatabiri kesho. Leo ni msingi wa kesho, kwa hivyo, kama ilivyo leo, hakuna mtu anayeweza kuyaelewa maneno ya Mungu kikamilifu. Ni baada tu ya maneno Yake kutimizwa kikamilifu ndipo wanadamu wataweza kuyaelewa kikamilifu.

Roho wa Mungu anajaza nafasi yote katika ulimwengu, lakini Yeye pia hufanya kazi ndani ya watu wote. Hivyo, katika mioyo ya watu, ni kana kwamba umbo la Mungu liko kila mahali na kila mahali pana kazi ya Roho Wake. Kwa kweli, kusudi la kuonekana kwa Mungu katika mwili ni kuwashinda mifano hawa halisi wa Shetani na mwishowe kuwapata. Akiwa anafanya kazi katika mwili, hata hivyo, Roho pia anashirikiana na mwili kuwabadilisha watu hawa. Inaweza kusemwa kuwa matendo ya Mungu yanaenea katika ulimwengu mzima na kwamba Roho Wake anaujaza ulimwengu mzima, lakini kwa sababu ya hatua za kazi Yake, wale wanaofanya uovu hawajaadhibiwa, huku wale ambao hutenda mema hajatuzwa. Kwa hivyo, vitendo Vyake havijasifiwa na watu wote wa ulimwengu. Yeye yuko juu na ndani ya vitu vyote; aidha, Yeye yuko miongoni mwa watu wote. Hili linatosha kuonyesha kuwa Mungu hakika yupo. Kwa sababu hajawaonekana wanadamu wote waziwazi, wamekuwa na fikira za uwongo kama vile, “Kulingana na binadamu, Mimi kwa kweli nipo, lakini pia naonekana kutokuwepo.” Kati ya wale wote ambao sasa wanaamini katika Mungu, hakuna mtu aliye na uhakika kabisa, asilimia mia moja kwamba Mungu kwa kweli yupo; wote wanashuku asilimia sitini na kuamani asilimia arubaini. Hivi ndivyo wanadamu walivyo sasa. Watu wote siku hizi wako katika hali ifuatayo: Wanaamini kwamba kuna Mungu, lakini hawajamwona; au, hawaamini kuwa kuna Mungu,

lakini wana shida nyingi ambazo wanadamu hawawezi kutatua. Inaonekana kila wakati kuna kitu ambacho kinawashikilia ambacho hawawezi kukikimbia. Hata ingawa wanamwamini Mungu, inaonekana kwamba kila wakati wao huhisi ukosefu wa uyakini. Hata hivyo, ikiwa hawaamini, wanaogopa kupoteza iwapo itatukia kwamba Yupo. Hii ndiyo hisia yao kinzani.

“Kwa ajili ya jina Langu, kwa ajili ya Roho Wangu, na kwa sababu ya mpango Wangu mzima wa usimamizi, ni nani anayeweza kutoa nguvu zake zote?” Mungu pia alisema, “Leo, wakati ambao ufalme upo katika ulimwengu wa wanadamu, ni wakati ambao Nimekuja binafsi miongoni mwa binadamu. Je, kuna yeyote ambaye anaweza kujitokeza aende kwenye uwanja wa vita kwa niaba Yangu bila hofu yoyote?” Kusudi la maneno ya Mungu ni hili: Isingekuwa kwa sababu ya Mungu mwenye mwili kufanya kazi Yake ya kiungu moja kwa moja, au Yeye asingekuwa mwenye mwili lakini badala yake Afanye kazi kupitia wahubiri, basi Mungu asingeweza kamwe kulishinda joka kubwa jekundu, wala Asingeweza kamwe kutawala kama Mfalme miongoni mwa wanadamu. Wanadamu wasingeweza kumjua Mungu Mwenyewe katika uhalisi, kwa hivyo huu bado ungekuwa utawala wa Shetani. Hivyo, hatua hii ya kazi lazima ifanywe na Mungu binafsi, kupitia katika mwili. Kama mwili ungebadilishwa, basi hatua hii ya mpango haingekamilika kamwe, kwa sababu umuhimu na kiini cha mwili ulio tofauti visingekuwa sawa. Watu wanaweza tu kuelewa maana halisi ya maneno haya, kwa sababu Mungu huelewa kiini. Mungu alisema, “Hata hivyo, baada ya yote, hakuna mtu anayeelewa ikiwa hii ni kazi ya Roho au ni kazi ya mwili. Itawachukua watu maisha yote kupitia jambo hili moja.” Watu wamepotoshwa na Shetani kwa miaka mingi sana, na walipoteza ufahamu wao wa mambo ya kiroho zamani. Kwa sababu hii, sentensi moja tu ya maneno ya Mungu ni kama karamu kwa macho ya watu. Kwa sababu ya umbali kati ya Roho na mapepo, wale wote wamwaminio Mungu wanahisi hisia ya kumtamani sana, na wote wako tayari kuwa karibu na Yeye na kumimina mioyo yao. Hata hivyo, hawathubutu kuwasiliana na Yeye, na badala yake wanabaki wakistahi. Hii ni nguvu ya kuvutia inayomilikiwa na Roho. Kwa sababu Mungu ni Mungu wa kupendwa na watu, na ndani Yake kuna vitu visivyo na mwisho vya wao kupenda, kila mtu anampenda na kila mtu anatamani kumwambia siri. Kwa kweli, kila mtu ana upendo kwa Mungu moyoni mwake—ni kwamba tu vurugu ya Shetani imewazuia watu wasiohisi, wapumbavu, wenye kuhurumiwa kumjua Mungu. Hii ndiyo sababu Mungu alizungumza juu ya hisia za kweli ambazo wanadamu wanazo Kwake: “Wanadamu hawajawahi kunichukia ndani ya vina vya mioyo yao; badala yake, wananishikilia katika vina vya roho zao. ... Uhalisi Wangu unawaacha wanadamu wasijue la kufanya, wakipigwa na butwaa na kukanganyikiwa, na bado wako tayari kuukubali.” Hii ndiyo hali halisi ndani kabisa ya mioyo ya wale wanaomwamini Mungu. Watu wanapomjua Mungu kweli, mtazamo wao Kwake hubadilika kwa kawaida, na wanaweza kutamka sifa kutoka ndani ya vina vya mioyo yao kwa sababu ya kazi ya roho zao.

Mungu yuko ndani ya vina vya roho za watu wote, lakini kwa sababu ya upotoshaji wa Shetani, watu wamekanganyikiwa kujua tofauti kati ya Mungu na Shetani. Kazi ya Mungu leo inanza na shida hii hasa, na katika ulimwengu wa kiroho, imekuwa lengo la vita tangu mwanzo hadi mwisho.

Sura ya 16

Kwa watu, Mungu ni mkuu mno, mwenye utele mno, wa ajabu mno, Asiyeeleweka mno; machoni pao, maneno ya Mungu hupaa juu, na huonekana kama kazi bora sana ya ulimwengu. Lakini kwa vile watu wana kasoro nyingi sana, na akili zao ni za kawaida sana, na, zaidi ya hayo, kwa kuwa uwezo wao wa kukubali ni haba mno, bila kujali vile Mungu hunena maneno Yake kwa dhahiri, wanabaki palepale bila kutikisika, kana kwamba wana ugonjwa wa akili. Wanapokuwa na njaa, hawaelewi kwamba lazima wale, wanapokuwa na kiu, hawaelewi kwamba lazima wanywe maji; wanaendelea tu kupaaaza sauti na kupiga yowe, kana kwamba kuna dhiki isiyoelezeka katika kina cha roho zao, lakini hawawezi kuzungumza kuihusu. Mungu alipowaumba wanadamu, kusudi Lake lilikuwa mwanadamu aishi katika ubinadamu wa kawaida na akubali maneno ya Mungu kulingana na silika yake. Lakini kwa kuwa, mwanzoni kabisa, mwanadamu alishindwa na majaribu ya Shetani, leo anabakia asiyeweza kujinasua, na bado hawezi kutambua hila za udanganyifu ambazo zimetetelezwa na Shetani kwa maelfu ya miaka, zaidi ya hayo anakosa akili ya kuyajua maneno ya Mungu kwa ukamilifu—haya yote yamesababisha hali ya sasa. Kama yalivyo mambo leo, watu bado wanaishi katika hatari ya majaribu ya Shetani, na hivyo wanabaki wasioweza kufahamu kabisa maneno ya Mungu. Katika tabia za watu wa kawaida hakuna uhalifu au udanganyifu, watu wana uhusiano wa kawaida kati yao, hawafanyi mambo pekee yao, na maisha yao si duni wala ya kufifia. Kwa hiyo, vilevile, Mungu huinuliwa miongoni mwa wote, maneno Yake hupenya miongoni mwa wanadamu, watu huishi katika amani kati yao na chini ya utunzaji na ulinzi wa Mungu, dunia imejaa upatanifu, bila kuingilia kwa Shetani, na utukufu wa Mungu huwa na umuhimu mkuu sana miongoni mwa wanadamu. Watu kama hao ni kama malaika: watakatifu, wa kulisimua, wasiolalamika kamwe kuhusu Mungu, na hutoa juhudi zao zote kwa utukufu wa Mungu duniani pekee. Sasa ni wakati wa usiku wa giza, wote wanapapasa huku na huko na kutafuta, usiku wa giza kuu unawafanya wawe na woga, na hawana budi ila kutetemeka; wakisikiliza kwa makini, ngurumo za dhoruba baada ya dhoruba za upepo wa kaskazimagharibi unaonekana kuandamana na mamia ya kuomboleza ya mwanadamu. Watu huhuzunika na kulia kwa ajili ya majaliwa yao. Ni kwa nini wao husoma maneno ya Mungu lakini hawawezi kuyaelewa? Ni kana kwamba maisha yao yanakaribia kukosa tumaini, kana kwamba kifo kiko karibu kuwafika, kana kwamba siku yao ya mwisho iko mbele yao. Hali kama hizo za kusikitisha ndizo nyakati ambazo malaika dhaifu humwita Mungu, wakimwambia kuhusu dhiki zao wenyewe katika kilio kimoja chenye majonzi

baada ya kingine. Ni kwa sababu hii ndio malaika wanaofanya kazi miongoni mwa wana na watu wa Mungu hawatashuka kamwe juu ya mwanadamu tena; hili ni kuwazuia kupatikana katika kutawala kwa Shetani wakati wapo katika mwili, wasiweze kujinasua, na kwa hiyo wao hufanya tu kazi katika ulimwengu wa kiroho usioonekana kwa mwanadamu. Hivyo, Mungu anaposema “wakati ambapo Nitapanda hadi kwa kiti cha enzi katika moyo wa mwanadamu utakuwa wakati ambapo wana na watu Wangu wataitawala dunia,” Ananena kuhusu wakati ambapo malaika walio duniani wanafurahia baraka ya huduma kwa Mungu mbinguni. Kwa kuwa mwanadamu ni onyesho la roho za malaika, Mungu asema kwamba kwa mwanadamu, kuwa duniani ni kama kuwa mbinguni, yeye kumhudumia Mungu duniani ni kama malaika kumhudumia Mungu mbinguni moja kwa moja—na hivyo, wakati wa siku zake duniani, mwanadamu hufurahia baraka za mbingu ya tatu. Hili ndilo hasa linasemwa katika maneno haya.

Kuna maana nyingi iliyofichwa katika maneno ya Mungu. “Siku itakapokuja, watu watanijua Mimi ndani kabisa ya nyoyo zao, na watakuja kunikumbuka Mimi kwenye mawazo yao” inaelekezwa kwa roho ya mwanadamu. Kwa sababu ya udhaifu wa malaika, wao humtegemea Mungu kila mara katika mambo yote, na kila mara wamempenda Mungu na kumsujudu. Lakini kwa sababu ya usumbufu wa Shetani, hawawezi kujisaidia, hawawezi kujidhibiti, wanataka kumpenda Mungu lakini hawawezi kumpenda kwa mioyo yao yote, na kwa hivyo wao hupatwa na maumivu. Ni wakati tu ambapo kazi ya Mungu inafika kiwango fulani ndio hamu ya malaika hawa ya kumpenda Mungu kweli inaweza kutimia, ndio maana Mungu alinena maneno hayo. Asili ya malaika ni kupenda, kuhifadhi kwa upendo mkubwa, na kumtii Mungu, lakini hawajaweza kutimiza hili duniani, na hawajakuwa na budi ila kustahimili mpaka wakati huu. Unaweza kuuangalia ulimwengu wa leo: Kuna Mungu ndani ya mioyo ya watu wote, lakini watu hawana uwezo wa kutofautisha iwapo Mungu aliye mioyoni mwao ni Mungu wa kweli au ni mungu wa uwongo, na ingawa wanampenda huyu Mungu wao, hawawezi kumpenda Mungu kweli, ambalo linamaanisha hawana uwezo wa kujidhibiti. Sura mbaya ya mwanadamu iliyofichuliwa na Mungu ni sura halisi ya Shetani katika ulimwengu wa kiroho. Mwanadamu alikuwa maasumu kwa asili, na bila dhambi, na hivyo tabia zote potovu, mbaya za mwanadamu ni matendo ya Shetani katika ulimwengu wa kiroho, na ni rekodi ya kweli ya maendeleo ya ulimwengu wa kiroho. “Leo, watu wamehitimu, na wanaamini wanaweza kutembea kwa maringo mbele Yangu, na kucheka na kufanya mzaha na Mimi bila kizuizi hata kidogo, na kunihutubia Mimi kama wenzao. Bado mwanadamu hanijui Mimi, bado anaamini kuwa kiasili sisi ni kama tuko sawa, kuwa sisi sote ni wa nyama na damu, na sote tunaishi kwenye dunia ya binadamu.” Hiki ndicho ambacho Shetani amefanya ndani ya moyo wa mwanadamu. Shetani hutumia dhana na macho ya mwanadamu kumpinga Mungu, lakini bila kupotosha watu Mungu huwaambia watu kuhusu matukio haya ili mwanadamu aweze kuepuka

balaa hapa. Udhaifu wa kufisha wa watu wote ni kwamba wao huona tu “mwili wa nyama na damu, na hawamtambui Roho wa Mungu.” Huu ni msingi wa hali moja ya ushawishi wa Shetani kwa mwanadamu. Watu huamini kwamba Roho aliye katika mwili huu pekee ndiye Anaweza kuitwa Mungu. Hakuna mtu anayeamini kwamba leo, Roho amepata mwili na Ameonekana kwa kweli machoni pao; watu humwona Mungu kama sehemu mbili—“vazi na mwili”—na hakuna yeyote anayemwona Mungu kama kupata mwili kwa Roho, hakuna yeyote anayeona kwamba kiini cha mwili ni tabia ya Mungu. Katika mawazo ya watu, Mungu ni wa kawaida hasa, lakini hawajui kwamba katika ukawaida huu hali moja ya umuhimu mkuu wa Mungu imejificha ndani.

Mungu alipoanza kuufunika ulimwengu wote, uligeuka kuwa giza totoro, na watu walipolala, Mungu alichukua nafasi hii kushuka miongoni mwa wanadamu, na Akaanza rasmi kutoa Roho kwa kila pembe ya dunia, Akaanza kazi ya kuwaokoa wanadamu. Inaweza kusemwa kwamba wakati ambapo Mungu alianza kuchukua mfano wa mwili, Mungu alifanya kazi duniani Mwenyewe. Kisha kazi ya Roho ikaanza, na hapo kazi yote duniani ikaanza rasmi. Kwa miaka elfu mbili, Roho wa Mungu amefanya kazi kotekote ulimwenguni. Watu hawalijui wala kulihisi hili, lakini wakati wa siku za mwisho, wakati ambapo enzi hii inakaribia kuhitimishwa, Mungu tayari ameshuka duniani kufanya kazi Mwenyewe. Hii ni baraka ya wale waliozaliwa wakati wa siku za mwisho, ambao wanaweza kutazama wenyewe mfano wa Mungu anayeishi katika mwili “Wakati uso wote wa undani ulikuwa na kiza, miongoni mwa wanadamu Nilianza kuonja uchungu wa dunia. Roho Yangu husafiri kote duniani na kuangalia ndani ya nyoyo za watu wote, licha ya hayo, pia, Mimi hushinda mwanadamu katika nyama ya kuwa mwili Kwangu.” Ushirikiano wa upatanifu kati ya Mungu aliye mbinguni na Mungu aliye duniani ni kama huo. Hatimaye, katika fikira zao watu wataamini kwamba Mungu aliye duniani ni Mungu aliye mbinguni, kwamba mbingu na dunia na vitu vyote ndani mwao viliumbwa na Mungu aliye duniani, kwamba mwanadamu anadhibitiwa na Mungu aliye duniani, kwamba Mungu aliye duniani huifanya kazi iliyo mbinguni hapa duniani, na kwamba Mungu aliye mbinguni Ameonekana katika mwili. Hili ndilo lengo kuu la kazi ya Mungu duniani, na kwa hiyo, hatua hii ni kiwango cha juu zaidi cha kazi katika kipindi cha mwili, na inatekelezwa katika uungu, na husababisha watu wote kuridhika kwa kweli. Kadri watu wanavyomtafuta Mungu katika dhana zao, ndivyo wanavyohisi zaidi kwamba Mungu aliye duniani si halisi. Hivyo, Mungu asema kwamba watu humtafuta Mungu miongoni mwa maneno matupu na mafundisho ya dini. Kadri watu wanavyomjua Mungu katika dhana zao, ndivyo wanavyokuwa stadi zaidi katika kunena maneno haya na mafundisho ya dini, na ndivyo wanavyokuwa wa ajabu zaidi; kadri watu wanavyonena maneno na mafundisho ya dini, ndivyo wanavyopotea zaidi kutoka kwa Mungu, na ndivyo wasivyoweza kujua zaidi kiini cha mwanadamu, na ndivyo wanavyomuasi Mungu zaidi, na ndivyo wanavyoondoka zaidi kwa matakwa ya Mungu. Matakwa ya Mungu kwa

mwanadamu si ya ajabu kama wanavyodhani watu, lakini kamwe hakuna yeyote ambaye amewahi kuelewa kweli mapenzi ya Mungu, na hivyo Mungu asema, “watu hutafuta tu katika anga isiyokuwa na mipaka, au juu ya bahari ambayo si tulivu, au juu ya ziwa tulivu, au miongoni mwa barua na mafundisho tupu.” Kadri Mungu anavyomwekea mwanadamu matakwa mengi, ndivyo watu wanavyohisi zaidi kwamba Mungu hafikiki, na ndivyo wanavyoamini zaidi kwamba Mungu ni mkuu. Hivyo, katika fahamu yao, maneno yote yanayonenwa kutoka kinywani mwa Mungu hayafikiwi na mwanadamu, kumfanya Mungu asiwe na budi ili kutenda mwenyewe; mwanadamu, wakati ule ule, hana mwelekeo hata kidogo wa kushirikiana na Mungu, na anashikilia tu kuinamisha kichwa chake na kukiri dhambi zake, akijaribu kuwa mnyenyekevu na mtiifu. Kwa hivyo, bila kutambua, watu huingia katika dini mpya, katika utaratibu wa dini ulio ni wa juu zaidi kuliko ule ulio katika makanisa ya dini. Hili linahitaji kwamba watu warudi katika hali za kawaida kupitia ugeuzaji wa hali yao hasi kuwa ile ya kujenga; la sivyo, mwanadamu daima atakuwa aliyetegwa mno.

Kwa nini Mungu husisitiza kueleza milima na maji katika matamko Yake ya nyakati nyingi? Je, kuna maana ya ishara katika maneno haya? Mungu hamruhusu tu mwanadamu kuyaona matendo Yake katika mwili Wake, bali pia Hamruhusu mwanadamu kuelewa nguvu Zake katika anga. Kwa njia hii, na wakati huo huo kuamini bila shaka kwamba huyu ni Mungu katika mwili, watu pia huja kuyajua matendo ya Mungu wa vitendo, na hivyo Mungu aliye duniani anatumwa kwenda mbinguni, na Mungu aliye mbinguni analetwa duniani, ni baada ya hapo tu ndipo watu wanaweza kuona kabisa kile Mungu alicheo na kupata ufahamu mkuu zaidi wa kudura ya Mungu. Kadri Mungu anavyoweza kuwashinda wanadamu katika mwili na kuupita mwili na kusafiri juu na kila pahali katika ulimwengu mzima, ndivyo watu wanavyoweza kuyaona matendo ya Mungu zaidi kwa msingi wa kumwona Mungu wa vitendo, na hivyo kujua kweli ya kazi ya Mungu kote kote katika ulimwengu mzima, kwamba si ya uwongo bali halisi, na hivyo wanakuja kujua kwamba Mungu wa vitendo wa leo ni mfano halisi wa Roho, na sio wa aina moja ya mwili kama wa mwanadamu. Hivyo, Mungu asema, “Lakini Ninapoamua kutoa ghadhabu Yangu, milima hupasuliwa vipande mbalimbali mara moja, ardhi huanza kutetemeka mara moja, maji hukauka mara moja, na mwanadamu huzingirwa na maafa mara moja.” Watu wanaposoma neno la Mungu, wanayahusisha na mwili wa Mungu, na hivyo, kazi na maneno katika ulimwengu wa kiroho yanaelekea moja kwa moja kwa Mungu wa mwili, ambalo linazidisha kufaa. Mungu anaponena, mara nyingi huwa ni kutoka mbinguni kuelekea duniani, na tena kutoka duniani kuelekea mbinguni, watu wote wakiachwa wasiweze kuelewa motisha na asili za maneno ya Mungu. “Ninapokuwa miongoni mwa mbingu, kamwe nyota hazijawahi kutishiwa na kuwepo Kwangu. Bali, huwa zinaweka nyoyo zao kunifanyia kazi Mimi.” Hali ya mbinguni ni kama hii. Mungu hupanga kwa utaratibu kila kitu katika mbingu ya tatu, na watumishi wote

wanaomhudumia Mungu wakimfanyia Mungu kazi yao wenyewe. Hawajawahi kufanya chochote kumuasi Mungu, kwa hiyo hawaingii katika wasiwasi unaozungumziwa na Mungu, lakini badala yake wanafanya kazi zao kwa dhati, kamwe hakuna mchafukoge wowote, na hivyo malaika wote huishi katika nuru ya Mungu. Wakati ule ule, kwa sababu ya uasi wao, na kwa sababu hawamjui Mungu, watu wote duniani huishi gizani, na kadri wanavyompinga Mungu, ndivyo wanavyoishi gizani zaidi. Mungu anaposema, “Kila mbingu inapong’aa zaidi, ndivyo dunia chini yake inazidi kuwa na giza,” Ananena kuhusu vile siku ya Mungu inakaribia zaidi na zaidi kwa wanadamu wote. Hivyo, shughuli ya Mungu ya miaka 6,000 katika mbingu ya tatu itahitimishwa hivi punde. Vitu vyote duniani vimeingia katika sura ya mwisho, na hivi punde kila kimoja kitaondolewa mkononi mwa Mungu. Kadri watu wanavyoenda mbali zaidi na kipindi cha siku za mwisho, ndivyo wanavyoweza kuonja zaidi upotovu katika ulimwengu wa mwanadamu; na kadri wanavyoenda mbali zaidi na siku za mwisho, ndivyo wanavyofurahisha miili yao; hata kuna wengi ambao wanataka kugeuza hali ya kusikitisha ya ulimwengu, lakini wote hukata tamaa katikati ya tanafusi zao kwa ajili ya matendo ya Mungu. Hivyo, watu wanapohisi joto la majira ya kuchipua, Mungu huyafunika macho yao, na kwa hiyo wao huelewa juu ya mawimbi yanayopanda na kushuka, hakuna hata mmoja wao anaweza kufikia mashua ya kuokoa maisha iliyo mbali. Kwa kuwa watu ni wadhaifu kwa asili, Mungu asema hakuna wowote wanaoweza kuyaboresha mambo. Watu wanapokata tamaa, Mungu huanza kunena kwa ulimwengu mzima, Anaanza kuwaokoa wanadamu wote, na ni baada ya hili tu ndipo watu wanaweza kufurahia maisha mapya yanayokuja baada ya mambo kuboreshwa. Watu wa leo wako katika hatua ya kujidanganya. Kwa kuwa njia iliyo mbele yao ni ya kuhuzunisha mno, na si dhahiri, na siku zao za baadaye ni “bila kikomo” na “bila mipaka,” watu wa enzi hii hawana mwelekeo wa kupigana, na wanaweza tu kupitisha siku zao kama ndege aitwaye Hanhao.^[a] Kamwe hakujawahi kuwa na mtu yeyote ambaye ameyafuatilia maisha kwa makini, na kufuatilia ufahamu wa maisha ya mwanadamu; badala yake, wanangoja siku ambayo Mwokozi aliye mbinguni atashuka ghafula kugeuza hali ya kusikitisha ya ulimwengu, ni baada ya hapo tu ndio watakuwa wenye ari katika majaribio yao kuishi. Hivyo ndivyo ilivyo hali ya kweli ya wanadamu wote na fikira ya watu wote.

Leo, Mungu anatabiri maisha mapya ya mwanadamu ya siku za baadaye kulingana na fikira zake wakati huu, ambayo ni dalili ya nuru ambayo Mungu anazungumzia. Kile ambacho Mungu anatabiri ni kile ambacho hatimaye kitatimizwa na Mungu, na ni matokeo mazuri ya ushindi wa Mungu dhidi ya Shetani. “Nasonga juu ya wanadamu wote na Natazama kila mahali. Hakuna kinachokaa kizee kamwe, na hakuna mtu ambaye yuko kama alivyokuwa. Ninapumzika katika kiti cha enzi, Naegemea juu ya ulimwengu mzima....” Haya ni matokeo ya kazi ya Mungu ya sasa. Wateule wote wa Mungu wanarudi kwa umbo lao la asili, kwa sababu hiyo malaika, ambao

wameteseka kwa miaka mingi sana, wanaachiliwa, kama tu asemavyo Mungu, “kila mmoja akiwa na uso kama wa mtakatifu ndani ya moyo wa binadamu.” Kwa sababu malaika hufanya kazi duniani na kumhudumia Mungu duniani, na utukufu wa Mungu husambaa kila mahali ulimwenguni, mbingu inaletwa duniani, na dunia inainuliwa kwenda mbinguni. Kwa hivyo, mwanadamu ni kiungo kinachounganisha mbingu na dunia; mbingu na dunia haziko mbali tena, hazijatengana tena, lakini zimeunganishwa kama kitu kimoja. Kote kote ulimwenguni, Mungu na mwanadamu ndio pekee wanaoishi. Hakuna vumbi wala uchafu, na vitu vyote vinafanywa upya, kama mwanakondoo mdogo anayelala katika ukanda wa mbuga wa kijani kibichi chini ya anga, akifurahia neema yote ya Mungu. Na ni kwa sababu ya ujio wa kijani kibichi ndiposa pumzi ya uhai inaangaza, kwani Mungu anakuja duniani kuishi pamoja na mwanadamu milele yote, kama ilivyosemwa kutoka kinywani mwa Mungu kwamba “Ninaweza kukaa kwa amani ndani ya Zayuni tena.” Hii ni ishara ya kushindwa kwa shetani, ni siku ya pumziko la Mungu, na siku hii itatukuzwa na kutangazwa na watu wote, na itafanyiwa kumbukumbu na watu wote. Wakati ambapo Mungu ametulia juu ya kiti cha enzi pia ndio wakati ambapo Mungu anahitimisha kazi Yake duniani, na ndio wakati ule ambao siri zote za Mungu zinaonyeshwa kwa mwanadamu; Mungu na mwanadamu watakuwa katika upatanifu daima, hawatakuwa mbali tena—haya ni mandhari mazuri ya ufalme!

Katika siri zimefichwa siri, na maneno ya Mungu ni ya kina kweli na yasiyoeleweka!

Tanbihi:

a. Hadithi ya ndege wa Hanhao inafanana sana na hekaya ya Aesop ya mchwa na panzi. Ndege wa Hanhao hupenda zaidi kulala kuliko kujenga kiota wakati hali ya hewa ni ya vuguvugu, licha ya onyo la marudio kutoka kwa jirani wake, ndege wa jamii ya kunguru. Wakati majira ya baridi hufika, ndege huyo huganda hadi kifo.

Sura ya 17

Kwa kweli, maneno yote kutoka katika kinywa cha Mungu ni mambo ambayo wanadamu hawayajui; yote ni lugha ambayo watu hawajasikia, kwa hiyo inaweza kusemwa hivi: Maneno ya Mungu yenyewe ni siri. Watu wengi kwa kutojua wanaamini kwamba ni mambo tu ambayo watu hawawezi kutimiza kimawazo, mambo ya mbinguni ambayo Mungu anawawezesha watu kuyajua sasa, au ukweli kuhusu kile Mungu anachofanya katika ulimwengu wa kiroho ni siri. Hili linaonyesha kwamba watu hawachukulii maneno yote ya Mungu kwa usawa, wala hawayathamini, lakini wanalenga kile wanachoamini kuwa “siri.” Hili linathibitisha kwamba watu hawajui maneno ya Mungu ni nini au siri ni nini—wao husoma tu maneno ya Mungu kutoka kwa fikira zao wenyewe. Ukweli ni kwamba hakuna hata mtu mmoja ambaye anapenda maneno ya Mungu kweli—kiini cha kwa nini inasemwa kwamba “Watu ni mabingwa wa kunihadaa Mimi” iko papa hapa. Hakika si kwamba Mungu anasema watu hawana ustahili

wowote, au kwamba wao ni takataka kabisa. Hii ndiyo hali halisi ya wanadamu. Watu wenyewe hawaelewi vyema kuhusu kiasi gani Mungu anamiliki katika mioyo yao—Mungu Mwenyewe pekee ndiye Anajua kwa ukamilifu. Kwa hiyo sasa hivi watu wanafanana na watoto wadogo wanyonyao—hawajui kabisa kwa nini wanakunywa maziwa na kile wanachoishia. Ni mama yao tu anayefahamu mahitaji yao, hatawaruhusu kufa njaa, wala hatawaruhusu kula chakula kingi kupindukia. Mungu anajua mahitaji ya watu bora zaidi, kwa hiyo wakati mwingine upendo Wake hujumuishwa katika maneno Yake, wakati mwingine hukumu Yake hufunuliwa ndani ya maneno hayo, wakati mwingine maneno Yake huumiza mioyo ya ndani kabisa ya watu, na wakati mwingine maneno Yake ni ya kweli sana na ya dhati. Hii huwaruhusu watu kuhisi fadhili Zake na upatikanaji Wake, na kwamba Yeye si “mtu wa kulazimisha” ambaye Anafikiriwa, Yule ambaye hawezi kuguswa, wala Yeye si “Mwana wa Mbinguni” katika akili za watu, ambaye Hawezi kutazamwa moja kwa moja usoni, na hasa Yeye si “muuaji” Ambaye watu wanadhani Huwaua wasio na hatia. Tabia yote ya Mungu imefunuliwa katika kazi Yake, tabia ya Mungu aliye katika mwili leo bado inajumuishwa kupitia kwa kazi Yake, kwa hiyo huduma ambayo Mungu huifanya ni huduma ya maneno, si kile Anachofanya au jinsi Anavyoonekana nje. Mwishowe watu wote watapata ujenzi wa maadili kutoka kwa maneno ya Mungu na kufanywa kamili kwa sababu ya maneno hayo. Katika uzoefu wao, kwa sababu ya uongozi wa maneno ya Mungu, watapata njia ya kufanya mazoezi, na kupitia maneno kutoka katika kinywa cha Mungu watu watajua tabia Yake yote. Kwa sababu ya maneno hayo kazi yote ya Mungu itatimizwa, watu watachangamka, na maadui wote watashindwa. Hii ndiyo kazi ya msingi, na hakuna mtu anayeweza kuipuuza. Tunaweza hata hivyo kuangalia maneno Yake: “Sauti Yangu inatoka kama radi, ikitia nuru roboduara zote nne na dunia nzima, na katikati ya radi na umeme, binadamu wanaangushwa chini. Hakuna mwanadamu aliyewahi kusimama imara katikati ya radi na umeme: Wanadamu wengi wanaogopa sana kuja kwa mwangaza Wangu na hawajui cha kufanya.” Wakati Mungu anapokifungua kinywa Chake maneno hutoka tu. Yeye hufanikisha kila kitu kupitia kwa maneno, na vitu vyote vinabadilishwa kwa maneno Yake, watu wote wanafanywa upya kwa maneno Yake. Je, “radi na umeme” zinahusu nini? Na “nuru” inahusu nini? Hakuna kitu hata kimoja ambacho kinaweza kuepuka maneno ya Mungu. Anatumia maneno Yake kuweka wazi akili za watu na kuonyesha ubaya wao; Anatumia maneno kushughulikia asili ya kale ya watu na kuwafanya watu Wake wote wawe kamili. Je, huu sio umuhimu wa maneno ya Mungu? Katika ulimwengu mzima, ikiwa hapangekuwa na msaada na kutegemezwa kwa maneno ya Mungu, wanadamu wote wangekuwa wameangamizwa zamani kiasi cha kutokuwepo. Hii ni kanuni ya kile Mungu anachofanya, na ni mbinu ya kufanya kazi kwa mpango Wake wa usimamizi wa miaka elfu sita. Umuhimu wa maneno Yake unaweza kuonekana wazi kupitia kanuni hii. Maneno ya Mungu hupenya moja kwa moja katika kina cha nafsi za wanadamu. Mara tu wanapoonaa maneno Yake wanashangaa na kujawa na hofu na

kukimbia haraka. Wanataka kutoroka ukweli wa maneno Yake, ndiyo sababu “wakimbizi” hawa wanaweza kuonekana kila mahali. Baada tu ya maneno ya Mungu kutamkwa watu hutimua. Hii ni hali moja ya sura ya ubaya wa wanadamu ambayo Mungu anaonyesha. Hivi sasa, watu wote wanaamka polepole kutoka kwa mzubao wao. Ni kama kwamba hapo awali watu wote walikuwa wamepata kichaa, na sasa wanaona maneno ya Mungu na ni kama kwamba wana athari za kudumu baada ya ugonjwa huo na hawawezi kurejelea hali yao ya zamani. Hii ni hali halisi ya watu wote, na pia ni picha halisi ya sentensi hii: “watu wengi, wakiongozwa na huu mng’ao dhaifu, wanaamshwa mara moja kutoka kwa njozi zao. Lakini, hakuna aliyewahi kutambua kwamba siku imewadia mwangaza Wangu unaposhuka duniani.” Hii ndiyo maana Mungu alisema: “Wanadamu wengi wanashtuliwa na ujio wa ghafla wa mwangaza.” Kulisema hivi kunafaa kabisa. Maelezo ya Mungu kuhusu wanadamu hayatoi nafasi hata kidogo—kwa kweli Amefanya hili kwa usahihi na bila kosa, ndiyo sababu watu wote wameridhishwa kwa ukamilifu na bila kujua, upendo wao kwa Mungu umeanza kujengeka kutoka ndani kabisa ya mioyo yao. Kwa njia hii pekee ndiyo nafasi ya Mungu katika mioyo ya watu inazidi kabisa kuwa ya kweli, na hii pia ni njia mojawapo ambayo Mungu hufanya kazi.

“Wanadamu wengi wamechanganyikiwa tu; wamejeruhiwa machoni na kutupwa chini matopeni na mwangaza.” Kwa sababu wanaenda kinyume cha mapenzi ya Mungu (yaani, wanampinga Mungu), mtu wa aina hiyo hupitia kuadibu kwa sababu ya uasi wake wakati maneno ya Mungu yanakuja; hii ndiyo sababu inasemekana kwamba wamejeruhiwa machoni na mwangaza. Mtu wa aina hii tayari amepeanwa kwa Shetani, hivyo wakati anaingia katika kazi mpya hana nuru au mwangaza wowote. Wale wote ambao hawana kazi ya Roho Mtakatifu wamemilikiwa na Shetani, na ndani kabisa ya mioyo yao hakuna mahali pa Mungu, kwa hiyo inasemekana kwamba “wametupwa chini matopeni.” Wale ambao wako katika hali hii wote wako katika hali ya mchafukoge. Hawawezi kuingia katika njia sahihi, hawawezi kurudia tena hali ya kawaida, kile wanachofikiria katika akili zao yote ni kinyume. Watu wote duniani wamepotoshwa na Shetani kupita kiasi. Hawana uhai na wao wamejaa harufu ya maiti. Watu wote duniani wanaendelea kuishi katikati ya tauni ya viini vya maradhi na hakuna mtu anayeweza kuepuka. Hawana nia ya kuendelea kuishi duniani, lakini daima wanahisi kwamba kuna kitu kikubwa zaidi kitakachotendeka ili kuwasababisha watu wakione wenyewe, kwa hivyo watu wote wanajilazimisha kuendelea kuishi. Watu hawajakuwa na nguvu mioyoni mwao kwa muda mrefu, wanatumia tu matumaini yao yasiyoonekana kama nguzo ya kiroho, kwa hiyo wanashikilia tu vichwa vyao wenyewe wakitenda kama mwanadamu, ili kukamilisha siku zao duniani. Ni kama kwamba watu wote ni wana wa shetani mwenye mwili. Ndiyo maana Mungu alisema: “Dunia imefunikwa na vurugu, ikifanya mtazamo wa kusikitisha usiovumilika ambao, ukichunguzwa kwa kina, unamtesa mtu na huzuni nyingi.” Kwa sababu ya kuonekana kwa hali

hii Mungu alianza “kutawanya mbegu za Roho Wangu” kuelekea ulimwengu wote, na Alianza kutekeleza kazi Yake ya wokovu duniani kote. Ni kwa sababu ya kuendeleza kazi hii ndio Mungu alianza kumimina kila aina ya maafa, hivyo kuwaokoa wanadamu wenye mioyo migumu. Katika awamu za kazi ya Mungu, njia ya wokovu bado inachukua mtindo wa majanga tofauti, na hakuna yeyote ambaye amepotea anaweza kuyaepuka Ni mwisho tu ndio hali ya “kutulia kama mbingu ya tatu: Hapa viumbe vilivyo hai vikubwa na vidogo vinaishi pamoja kwa amani, bila kushiriki katika ‘migogoro ya mdomo na ulimi hata mara moja’” kuwa na uwezo wa kuonekana duniani. Hali moja ya kazi ya Mungu ni kuwashinda wanadamu wote na kuwapata watu waliochaguliwa kupitia kwa maneno Yake. Hali nyingine ni kuwashinda wana wote wa uasi kupitia kwa maafa mbalimbali. Hii ni sehemu moja ya kazi kubwa ya Mungu. Ni kwa njia hii tu ndio ufalme ulio hapa duniani ambao Mungu anataka unaweza kutimizwa kwa ukamilifu, na hii ni sehemu ya kazi ya Mungu ambayo ni kama dhahabu nzuri.

Daima Mungu anahitaji kwamba watu waelewe elimumwendo ya mbinguni. Wanaweza kulitimiza jambo hilo kweli? Ukweli ni kwamba, kwa kutegemea hali halisi za watu sasa, baada ya kupotoshwa na Shetani kwa zaidi ya miaka 5,900, hawawezi kulinganishwa na Petro na hivyo hawawezi tu kufanya hivyo. Hii ni mojawapo ya mbinu za kazi ya Mungu. Hangewafanya watu wasubiri kwa kukaa tu, lakini Angewahitaji kutafuta kwa vitendo. Ni kwa njia hii tu ndiyo Mungu atakuwa na fursa ya kufanya kazi ndani ya watu. Hili linaweza pia kuelezewa kidogo zaidi, la sivyo watu watakuwa tu na ufahamu wa juu juu. Baada ya Mungu kuwaumba wanadamu na kuwapa roho, Aliwaagiza kwamba ikiwa hawangemwita Mungu, basi hawangeweza kuunganishwa na Roho Wake na hivyo “televisheni ya setilaiti” kutoka mbinguni haingepokelewa duniani. Wakati Mungu hayupo tena katika roho za watu kuna kiti kitupu kinachoachwa wazi kwa ajili ya vitu vingine, na hivyo ndivyo Shetani anavyotwaa fursa hiyo kuingia ndani. Wakati watu wanapowasiliana na Mungu kwa mioyo yao, Shetani huingia katika hofu kubwa na huharakisha kuhepa. Kupitia wa vilio vya wanadamu Mungu huwapa kile wanachohitaji, lakini “Hakai” ndani yao kwanza. Yeye daima huwapa tu msaada kwa sababu ya vilio vyao na watu hupata ujasiri kutoka kwa nguvu hizo za ndani ili Shetani asithubutu kuja hapa “kucheza” apendavyo. Kwa njia hii, ikiwa watu daima wanaunganishwa na Roho wa Mungu, Shetani hathubutu kuja kuvuruga. Bila vurugu ya Shetani, maisha yote ya watu ni ya kawaida na Mungu ana fursa ya kufanya kazi ndani yao bila viziwi vyovyote. Kwa njia hii, kile Mungu anataka kufanya kinaweza kutimizwa kupitia kwa wanadamu. Kutokana na hili inaweza kujulikana kwa nini Mungu daima Amewahitaji watu wazidishe imani yao, na pia Amesema: “Natoa matakwa ya kufaa kulingana na kimo cha mwanadamu. Sijawahi kumweka yeyote kwa matatizo, wala Sijawahi kumtaka yeyote ‘kukamua damu yake’ ili kujiridhisha.” Watu wengi sana wanakanganywa na matakwa ya Mungu, wakisema, kwa kuwa watu hawana akili hiyo na

wamepotoshwa na Shetani kiasi cha kutotengenezeka tena, kwa nini Mungu anaendelea kutoa matakwa kwao? Je, Mungu hawaweki watu katika hali ngumu? Unapoona nyuso za watu za dhati, na kisha kuona mtazamo wao wenye kufedhehesha, huna budi kucheka. Ubaya mbalimbali wa watu ni wa kuchekesha sana—wakati mwingine wao ni kama mtoto anayependa kucheza, na wakati mwingine wao ni kama msichana mdogo akimwigiza “mama.” Wakati mwingine wao ni kama mbwa akimla panya. Mtu hajui iwapo anafaa kucheka au kulia wakati wa hali hizi zake mbaya, na mara nyingi kadri watu wanavyoshindwa kuelewa mapenzi ya Mungu, ndivyo wanavyozidi kustahili kuingia kwenye shida. Ndiyo sababu inaweza kuonekana kutoka kwa maneno ya Mungu, “Mimi ni Mungu anayelazimisha tu ukimya kwa viumbe?” Jinsi watu walivyo wajinga, na inaonyesha kwamba hakuna mtu anayeweza kuelewa mapenzi ya Mungu. Hata Akieleza mapenzi Yake ni nini, hawawezi kuyazingatia. Wanafanya tu kazi ya Mungu kulingana na mapenzi ya binadamu, hivyo wanawezaje kuelewa mapenzi Yake kwa njia hiyo? “Natembea duniani, Nikitawanya harufu Yangu nzuri kila mahali, nami Naacha umbo Langu kila mahali. Kila pahali panatingika kwa mvumo wa sauti Yangu. Watu kila mahali wanadumu kwa hamu ya mambo waliyozoea ya urembo wa mandhari ya jana, kwani binadamu wote wanakumbuka siku za nyuma.” Hii itakuwa hali wakati ufalme utaundwa. Kwa kweli, katika sehemu kadhaa Mungu ametabiri uzuri wa utambuzi wa ufalme, na kama wote utajumuishwa, ni picha kamili ya ufalme. Lakini watu hawaizingatii—wao huiangalia tu kama katuni.

Kwa sababu ya miaka elfu kadhaa ya kupotoshwa na Shetani, watu daima wameishi katika giza, hivyo hawana wasiwasi na giza wala hawaitamani nuru. Hii ndiyo imesababisha hili wakati nuru imefika leo: “wote wanakirihishwa na ujio Wangu, wote wanaufukuza mwangaza usije, kana kwamba Mimi ni adui ya mwanadamu mbinguni. Mwanadamu ananisalimu na mwangaza wa kujikinga machoni mwake.” Ingawa watu wengi wanampenda Mungu kwa moyo wa kweli, bado Hajaridhika na bado Anawashutumu wanadamu. Hili linawakanganya watu. Kwa sababu watu wanaishi katika giza, huduma yao kwa Mungu bado inafanywa kwa njia sawa na katika hali ya kukosa mwanga. Yaani, watu wote humtumikia Mungu kwa kutumia fikira zao wenyewe, na wakati Mungu anapokuja watu wote wako katika hali hii na hawawezi kumhudumia Mungu kwa kukubali nuru mpya, lakini wanatumia uzoefu wao wote kumhudumia. Mungu hapati furaha kutoka kwa “kujitolea” kwa wanadamu, hivyo nuru haiwezi kusifiwa na wanadamu katika giza. Hii ndiyo sababu Mungu alisema maneno yaliyo hapo juu; hii kabisa bila shaka sio kinyume na ukweli, na sio Mungu anayewadhulumu wanadamu, wala sio Yeye anayewakosea. Tangu uumbaji wa ulimwengu mpaka leo, hakuna hata mtu mmoja ambaye amewahi kuonja joto la Mungu—wamekuwa wakijikinga dhidi ya Mungu, wakiogopa sana kwamba Mungu atawaangusha, kwamba Atawaangamiza. Kwa hiyo kwa zaidi ya miaka hii 6,000 daima Mungu ametumia uchangamfu kwa kubadilishana na uaminifu wa watu, na daima Amewaongoza kwa

uvumilivu kila wakati. Hii ni kwa sababu watu ni dhaifu sana, na hawawezi kufahamu mapenzi ya Mungu kwa ukamilifu, na hawawezi kumpenda kwa moyo wote, kwa sababu hawana budi kuwa chini ya utawala wa hila wa Shetani. Lakini ingawa huu ni ukweli, Mungu bado Anavumilia, na wakati Anapovumilia hili hadi siku fulani, yaani, wakati Atakapoufanya upya ulimwengu, Yeye hatawatunza tena watu kama mama afanyavyo. Badala yake, Atawapa wanadamu adhabu inayofaa ndiyo sababu baada ya hayo kutakuwa na: “Maiti wanasongasonga juu ya bahari,” huku “mahali ambapo hakuna maji, wanadamu wengine bado wanafurahia, wakicheka na kuimba, ahadi ambazo Nimewapa.” Huu ndio ulinganishi kati ya hatima za wale ambao wanaadhibiwa na wale ambao wanapewa thawabu. “Juu ya bahari” inahusu kuzimu ya kuadibu kwa wanadamu ambako Mungu alizungumzia. Ni hatima ya Shetani, na ni “mahali pa kupumzika” ambapo Mungu amewaandalia wote wanaompinga Yeye. Daima Mungu ametaka upendo halisi wa wanadamu, ingawa watu hawajui hili na hawana hisia kwayo, na wanazidi kufanya kazi yao wenyewe. Kutokana na haya, katika maneno Yake yote, daima Mungu anahitaji vitu kutoka kwa watu na anelezea dosari zao, na anawaeleza njia ya kutenda, ili waweze kutenda kulingana na maneno haya. Mungu pia Amefafanua juu ya mtazamo Wake mwenyewe kwa watu: “Bado, Sijawahi kuchukulia mzaha maisha ya binadamu hata mmoja kana kwamba ni kitu cha kuchezea. Nachunguza machungu mwanadamu amechukua na kuelewa bei ambayo amelipa. Anaposimama mbele Yangu, Sitamani kumpata mwanadamu kwa kumshtua kwa nia ya kumwadibu, wala kumtakia na kutawaza kwake vitu visivyohitajika. Badala yake, wakati huu wote nimemchunga mwanadamu, na kumpa mwanadamu, wakati huu wote.” Watu wanapoyasoma maneno haya kutoka kwa Mungu, wao huhisi uchangamfu Wake mara moja: Kwa kweli, zamani Nimelipa gharama kwa Mungu lakini pia Nimemtendea kwa uzembe, na wakati mwingine Nimelalamika Kwake. Daima Mungu ameniongoza kwa maneno yake na Yeye huzingatia sana maisha yangu, lakini wakati mwingine Mimi hucheza nayo kama kwamba ni mwanasesere. Kwa kweli si haki. Mungu ananipenda sana, kwa hivyo kwa nini Siwezi kujitahidi vya kutosha? Wakati wanapofikiri juu ya jambo hili, watu hutaka kujipiga nyuso zao, au, kuhusu watu wengine, pua zao hata hutetemeka na wao hulia kwa sauti kubwa. Mungu anaelewa mioyo ya watu na Husema ifaavyo, na maneno haya machache ambayo si magumu wala mororo huhimiza upendo wa watu kwa ajili ya Mungu. Hatimaye, Mungu alitabiri mabadiliko katika kazi Yake wakati ufalme unapoanzishwa duniani: Wakati Mungu yupo duniani, watu wataweza kuwa huru kutokana na balaa na maafa na wataweza kufurahia neema, lakini wakati Anapoanza hukumu ya siku kuu, itakuwa wakati Anapoonekana kati ya watu wote, na kazi Yake yote duniani itakuwa imekamili kabisa. Wakati huo, kwa sababu siku imefika, itakuwa sawasawa na ilivyosema katika Biblia: “Yule aliye dhalimu, basi aendelee kuwa dhalimu; na yeye aliye mtakatifu, na awe mtakatifu bado.” Wasio haki watakuja kwa kuadibiwa, na watakatifu watakuja machoni pa kiti cha enzi. Hakuna hata mtu mmoja atakayeweza kupata upendeleo Wake, hata

wana na watu wa ufalme. Yote itakuwa haki ya Mungu, na yote itakuwa ufunuo wa tabia Yake. Hataonyesha kujihusisha kwa ajili ya udhaifu wa wanadamu kwa mara ya pili.

Sura ya 18

Maneno yote ya Mungu yana sehemu fulani ya tabia Yake. Tabia ya Mungu haiwezi kuonyeshwa kikamilifu katika maneno, jambo ambalo linatosha kuonyesha ni kiasi gani cha utajiri kilicho ndani Yake. Kile ambacho watu wanaweza kuona na kugusa ni, finyu, hata hivyo, kama ulivyo uwezo wa watu. Ingawa maneno ya Mungu ni dhahiri, watu hawawezi kuyaelewa kikamilifu. Chukua maneno haya kwa mfano: “Katika mwako wa umeme, kila mnyama hufichuliwa katika hali yake halisi. Hivyo pia, kama wameangaziwa na mwanga Wangu, mwanadamu amepata tena utakatifu aliokuwa nao wakati mmoja. Eh, dunia potovu ya zamani! Mwishowe, imeanguka na kutumbukia ndani ya maji machafu na, imezama chini ya maji, na kuyeyuka na kuwa tope!” Maneno yote ya Mungu yana nafsi Yake, na ingawa watu wote wanayajua maneno haya, hakuna ambaye amewahi kuelewa maana yake. Machoni pa Mungu, wote ambao humpinga ni adui Zake, yaani, wale ambao ni wa pepo wabaya ni wanyama. Kutokana na hili, mtu anaweza kuona hali ya kweli ya kanisa. Wanadamu wote wanaangaziwa na maneno ya Mungu, na katika mwanga huu, wanajichunguza bila kupitia karipio au kurudiwa au kupuuzwa moja kwa moja na wengine, bila kushurutishwa na njia zingine za kibinadamu za kufanya mambo, na bila wengine kutaja mambo. Kutoka katika “mtazamo wa hadubini”, wanaona waziwazi ni kiasi gani cha maradhi kilicho ndani yao kweli. Katika maneno ya Mungu, kila aina ya roho imeainishwa na kufichuliwa katika umbo lake la asili. Roho za malaika zinakuwa zenye nuru zaidi, na ndiyo maana ya maneno ya Mungu: “Mwanadamu amepata tena utakatifu aliokuwa nao wakati mmoja.” Maneno haya yametegemezwa kwa matokeo ya mwisho yaliyotimizwa na Mungu. Kwa sasa, bila shaka, matokeo haya hayawezi kutimizwa kikamilifu—ni jaribio tu la mwanzo, ambalo kwalo mapenzi ya Mungu yanaweza kuonekana. Maneno haya yanatosha kuonyesha kwamba idadi kubwa ya watu wataporomoka katika maneno ya Mungu na watahindwa katika mchakato wa hatua kwa hatua wa kutakaswa kwa watu wote. Hapa “kuyeyuka na kuwa tope” hakukinzani na Mungu kuuangamiza ulimwengu kwa moto, na “umeme” linarejelea ghadhabu ya Mungu. Mungu anapoachilia ghadhabu Yake kuu, ulimwengu mzima utapitia maafa ya kila aina kama matokeo, kama vile volkano kufoka. Ninaposimama juu kabisa ya angani, inaweza kuonekana kuwa duniani, maafa ya aina mbalimbali yanawakaribia wanadamu wote, yakikaribia kila siku. Nikiangalia chini kutoka juu, dunia inaonyesha mandhari mbalimbali kama yale yanayotangulia tetemeko la ardhi. Moto unaotiririka unasonga bila kupingwa, lava inatiririka kwa uhuru, milima inasonga, na mwanga wa baridi unametameta juu ya kila kitu. Dunia nzima imezama katika moto. Haya ndiyo mandhari ya Mungu akitoa ghadhabu Yake, na pia ndio wakati wa hukumu Yake. Wale wote ambao ni wa damu na nyama

hawataweza kutoroka. Hivyo, vita kati ya nchi na migogoro kati ya watu havitahitajika kuharibu ulimwengu mzima; badala yake, dunia “itafurahia yenyewe kwa kufahamu” katika chanzo cha kuadibu kwa Mungu. Hakuna mtu atakayeweza kuiepuka; kila mtu atapitia katika mateso haya. Baada ya hapo, ulimwengu mzima utanza tena kuangaza kwa miale takatifu na wanadamu wote wataanza tena maisha mapya. Na Mungu atakuwa Amepumzika juu ya ulimwengu na Atawabariki wanadamu wote kila siku. Mbingu haitakuwa na ukiwa usiovumilika, lakini itarudia nguvu ambayo haijawahi kuwa nayo tangu kuumbwa kwa ulimwengu, na kuja kwa “siku ya sita” itakuwa wakati Mungu atanza maisha mapya. Mungu na wanadamu wote wataingia katika pumziko na ulimwengu hautakuwa tena mchafu au wenye najisi, lakini utafanywa upya tena. Ndiyo maana Mungu alisema: “Dunia si kimya cha mauti na nyamavu tena, mbingu si ya ukiwa na yenye huzuni tena.” Katika ufalme wa mbinguni, hakujakuwa na udhalimu au hisia za kibinadamu, au tabia yoyote potovu ya wanadamu, kwa sababu usumbufu wa Shetani haupo hapo. “Watu” wote wanaweza kuelewa maneno ya Mungu, na maisha mbinguni ni maisha yaliyojaa furaha. Wote walio mbinguni wana hekima na heshima ya Mungu. Kwa sababu ya tofauti iliyoko kati ya mbingu na dunia, raia wa mbinguni hawaitwi “watu”; badala yake, Mungu huwaita “roho”. Maneno haya mawili yana tofauti muhimu—wale wanaoitwa “watu” sasa wamepotoshwa na Shetani, wakati “roho” hazijapotoshwa. Mwishowe, Mungu atawabadilisha watu wa duniani wawe viumbe wenye sifa za roho wa mbinguni, na kisha hawatakuwa tena chini ya vurugu ya Shetani. Hii ndiyo maana halisi ya maneno, “utakatifu Wangu umeenea katika kila pembe ya ulimwengu.” “Nchi katika hali yake ya asili ni miliki ya mbingu, na mbingu imeungana na nchi. Mwanadamu ni ugwe unaunganisha mbingu na nchi, na kwa sababu ya utakatifu wa mwanadamu, kwa ajili ya kufanywa upya kwa mwanadamu, mbingu haijafichwa tena kutoka kwa nchi, na nchi haiko kimya tena kwa mbingu.” Hili linasemwa kuhusu watu walio na roho za malaika, na wakati huu, “malaika” watakuwa tena na uwezo wa kuishi pamoja kwa amani na kupata tena hali yao ya awali, hawatagawanywa tena na mwili kati ya falme za mbingu na dunia. “Malaika” walio duniani wataweza kuwasiliana na malaika walio mbinguni, watu walio duniani watajua siri za mbinguni, na malaika walio mbinguni watajua siri za ulimwengu wa binadamu. Mbingu na dunia zitaunganishwa, na hakutakuwa na umbali kati yao. Huu ni uzuri wa utambuzi wa ufalme. Ni kile ambacho Mungu atakamilisha, na ndicho kitu ambacho wanadamu wote na roho hutamani sana. Lakini wale walio katika ulimwengu wa kidini hawajui chochote kuhusu hili. Wao wanamngojea tu Yesu Mwokozi aje juu ya wingu jeupe na Azichukue roho zao, na kuacha “taka” zikitapakaa kila mahali duniani (taka inarejelera maiti). Je, hii si fikira ambayo wanadamu wote wanayo? Hii ndiyo maana Mungu alisema: “Eh, dunia ya dini! Ingekosaje kuangamizwa na mamlaka Yangu duniani?” Kwa sababu ya ukamilishaji wa watu wa Mungu ulimwenguni, ulimwengu wa kidini utapinduliwa. Hii ndiyo maana ya kweli ya “mamlaka” ambayo Mungu alizungumzia. Mungu alisema: “Kunao wale ambao, katika siku

Yangu, hulifedhehesha jina Langu? Watu wote huelekeza macho yao ya heshima Kwangu, na wao hunililia kwa siri katika nyoyo zao.” Hili ndilo Alilosema juu ya matokeo ya uharibifu wa ulimwengu wa dini. Utatii kikamilifu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu kwa sababu ya maneno Yake, na hawatasubiri tena wingu jeupe lishuke chini au watazame angani, lakini badala yake watahindwa mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Ndiyo sababu ya maneno, “wao hunililia kwa siri katika nyoyo zao”—haya yatakuwa matokeo kwa ulimwengu wa dini, ambao Mungu atakushinda kikamilifu. Hii ndiyo maana ya uweza wa Mungu—kuwaangusha chini watu wote wa dini, waasi wakuu kati ya wanadamu, ili kwamba wasiyashikilie tena mawazo yao wenyewe kwamba waweze kumjua Mungu.

Ingawa maneno ya Mungu yametabiri uzuri wa ufalme mara kwa mara, yamesema juu ya hali zake mbalimbali na kuzielezea kwa mitazamo tofauti, bado hayawezi kueleza kikamilifu kila hali ya Enzi ya Ufalme kwa sababu uwezo wa watu wa kupokea umepungukiwa sana. Maneno yote ya matamko Yake yamenenwa, lakini watu hawajayaangalia ndani kupitia kwa kipiga picha za ndani, X-ray na hivyo wamepungukiwa na mwanga na ufahamu na hata wamekanganywa. Hii ni kasoro kubwa zaidi ya mwili. Ingawa ndani ya mioyo yao, watu wanataka kumpenda Mungu, wanampinga kwa sababu ya usumbufu wa Shetani, kwa hiyo mara kwa mara Mungu amegusa mioyo ya watu yenye ganzi na isiyoelewa ili wapate kufufuliwa. Yote ambayo Mungu hufunua ni ubaya wa Shetani, kwa hivyo kadiri maneno Yake yalivyo makali zaidi, ndivyo Shetani huaibika zaidi, ndivyo mioyo ya watu inavyokuwa wazi zaidi, na ndivyo upendo wa watu unavyozidi kuamshwa. Hivi ndivyo Mungu anavyofanya kazi. Kwa sababu Shetani amefunuliwa na kwa sababu ametambuliwa, hathubutu tena kumiliki mioyo ya watu, na hivyo malaika hawachokozwi tena. Kwa njia hii, ndio wanampenda Mungu kwa moyo na akili zao zote. Ni wakati huu tu ndipo inakuwa wazi kuona kwamba, katika hali zao halisi, malaika ni wa Mungu na wanampenda Yeye. Ni kwa njia hii tu ndiyo mapenzi ya Mungu yanaweza kutimizwa. “Ndani ya nyoyo zao, sasa kuna nafasi kwa ajili Yangu. Sitakumbana tena na chuki na kukataliwa miongoni mwa wanadamu, kwani kazi Yangu kubwa imekwisha tekelezwa, na haizuiliwi tena.” Hii ndiyo maana ya yale yaliyoelezwa hapo juu. Kwa sababu ya uchokozi wa Shetani, watu hawawezi kupata wakati wa kumpenda Mungu na daima wao hutatizwa na mambo ya ulimwengu na wanahadaiwa na Shetani kiasi kwamba wao hutenda wakiwa wamechanganyikiwa. Hii ndiyo maana Mungu amesema kuwa wanadamu “wameyapitia matatizo mengi sana ya maisha, dhuluma nyingi za ulimwengu, mageuko mengi sana ya ulimwengu wa binadamu, lakini sasa huishi katika nuru Yangu. Je, ni nani asiyelia kwa ajili ya dhuluma za jana?” Wakati ambapo watu wamesikia maneno haya, wanahisi kama kwamba Mungu ni mwenzao katika taabu, Anasikitika nao, na wakati huo, Anashiriki nao malalamiko yao. Wanahisi ghafla maumivu ya ulimwengu wa binadamu na kufikiri: “Hiyo ni kweli kabisa—

Sijawahi kufurahia chochote duniani. Tangu nitoke tumboni mwa mama yangu hadi sasa nimepitia maisha ya binadamu na sijawahi kupata kitu chochote, lakini nimeteseke sana. Yote ni tupu kweli! Na sasa nimepotoshwa sana na Shetani! Oh! Ikiwa si kwa ajili ya wokovu wa Mungu, wakati wa kifo changu unapokuja, je, sitakuwa nimeishi maisha yangu yote bila sababu? Je, Kuna maana yoyote kwa maisha ya binadamu? Si ajabu Mungu alisema kuwa kila kitu chini ya jua ni tupu. Kama Mungu hangenipa nuru leo, bado ningekuwa gizani. Jambo ovu lililoje!”

Wakati huu, wanakuwa na shaka moyoni mwao: “Ikiwa siwezi kupata ahadi ya Mungu nitawezaje kuendelea kuwa na uzoefu wa maisha?” Kila mtu anayesoma maneno haya atalia akiomba. Hivyo ndivyo ilivyo roho ya mtu. Itakuwa vigumu kwa mtu kusoma hili na asiwe na mjibizo wowote, isipokuwa awe mwenye akili pungwani. Kila siku, hufichua hali za watu wa kila aina. Wakati mwingine, Yeye hutoa malalamiko kwa niaba yao. Wakati mwingine Huwasaidia watu kushinda na kupitia kwa ufanisi katika mazingira fulani. Wakati mwingine, Anawatajia watu “mabadiliko” yao. La sivyo, watu wasingejua kiasi ambacho wamekua katika maisha. Wakati mwingine, Mungu huonyesha uzoefu wa watu kwa uhalisi, na wakati mwingine Huonyesha upungufu na makosa yao. Wakati mwingine, Yeye hufanya matakwa mapya kwao, na wakati mwingine Huonyesha kiwango ambacho kwacho wao wanamwelewa Yeye. Hata hivyo, Mungu amesema pia: “Nimesikia maneno ya dhati yakinanwa na watu wengi, simulizi kutoka kwa watu wengi sana kuhusu matukio machungu ya mateso waliyopitia; Nimeona wengi sana, katika dhiki kubwa sana, wakinipa utiifu wao bila kukosa, na Nimewatazama wengi sana, wakitembea kwenye njia yenye mabonde, wakitafuta suluhisho.” Haya ni maelezo ya wahusika wa kujenga. Katika kila tukio la “tamthilia ya historia binadamu” sit u kwamba kumekuwa na wahusika chanya lakini kumekuwa na wahusika hasi pia. Kwa hivyo, Mungu anafichua ubaya wa wahusika hawa hasi. Hivyo, ni kupitia tu tofauti yao na “wasaliti” ndio uaminifu usiokubali kushindwa na ujasiri usio na hofu wa “wanadamu wenye haki” unafichuliwa. Katika maisha ya watu wote kuna vipengele hasi na pia, bila ubaguzi, vipengele vya kujenga. Mungu hutumia vyote kufichua ukweli juu ya watu wote, ili wasaliti wainamishe vichwa vyao na kukubali dhambi zao, na ili, kukiwa na himizo, watu wenye haki wataendelea kuwa waaminifu. Matokeo ya maneno ya Mungu ni ya kina kirefu sana. Wakati mwingine, watu huyasoma na kisha kuangua kicheko wakati mwingine, huinamisha tu vichwa vyao na kunyamaza. Wakati mwingine wanakumbuka, wakati mwingine wanalia kwa uchungu na kukiri dhambi zao, wakati mwingine wao hupapasa, na wakati mwingine wanatafuta. Kwa jumla, kuna mabadiliko katika mijibizo ya watu kwa sababu ya hali tofauti ambamo Mungu ananena. Mtu anaposoma maneno ya Mungu, wakati mwingine watazamaji wanaweza hata kuamini kwa makosa kwamba mtu huyo ni mgonjwa wa akili. Chukua maneno haya kwa mfano: “Na hivyo, migogoro yenye ubishi duniani haipo tena, na, kufuatia kutolewa kwa maneno Yangu, ‘silaha’ mbali mbali za enzi ya sasa zimeondolewa.” Neno “silaha” pekee linaweza kuibua kicheko cha siku nzima, na kila

ambapo mtu kwa bahati anaweza kukumbuka neno “silaha”, atajichekea mwenyewe kwa nguvu. Si hivi ndivyo ilivyo? Unawezaje kukosa kucheka kwa ajili ya hili?

Unapocheka, usisahau kufahamu kile ambacho Mungu anataka kwa wanadamu, na usisahau kuona hali ya kweli ya kanisa: “Binadamu wote wamerudi katika hali ya kawaida na kuanza maisha mapya. Wakiishi katika mazingira mapya, idadi kubwa ya watu huangalia kandokando yao, wakiishi kana kwamba wameingia katika ulimwengu mpya kabisa, na kwa sababu ya hili, wanashindwa kubadilika mara moja katika mazingira yao ya sasa ama kuingia mara moja kwenye njia nyofu.” Hii ndiyo hali ya kweli ya kanisa sasa. Usiwe na hamu sana kuwafanya watu wote waingie mara moja kwenye njia sahihi. Punde kazi ya Roho Mtakatifu itakapokuwa imeendelea hadi hatua fulani, watu wote wataingia ndani yake bila kutambua. Unapofahamu kiini cha maneno ya Mungu, utajua Roho Wake amefanya kazi hadi kufikia hatua ipi. Mapenzi ya Mungu ni: “Mimi husimamia tu, kulingana na udhalimu wa mwanadamu, kipimo mwafaka cha ‘elimu,’ bora ili kumwezesha kila mtu kushika njia nyofu.” Hii ni mbinu ya Mungu ya kuzungumza na kufanya kazi, na pia ndiyo njia mahsusi ya kutenda kwa wanadamu. Baada ya hili, Aliwaashiria watu hali nyingine za binadamu: “Kama wanadamu hawataki kufurahia upeo wa furaha iliyo ndani Yangu, Ninaweza kukubaliana tu na kile ambacho mioyo yao inatamani kufanya na kuwatupa katika shimo lisilo na mwisho.” Mungu alinena kwa ukamilifu na kuwaacha watu bila fursa hata kidogo ya kulalamika. Hii hasa ndiyo tofauti iliyopo kati ya Mungu na mwanadamu. Daima Mungu huzungumza na mwanadamu waziwazi na kwa uhuru. Katika kila kitu ambacho Mungu anasema, mtu anaweza kuuona moyo Wake wa dhati, unaowasababisha watu waipime mioyo yao dhidi ya Wake na kuwawezesha kuifungua mioyo yao Kwake, ili Aweze kuona hali zao halisi hasa. Mungu hajawahi kusifu imani ya mtu au upendo wa mtu yeyote, lakini daima Ametoa matakwa kwa watu na kufunua upande wao mbaya. Hii inaonyesha “kimo” kidogo walicho nacho watu na jinsi “katiba” yao ilivyo na upungufu. Wanahitaji “mazoezi” zaidi ili kufidia mapungufu haya, ndiyo maana kila wakati Mungu “huwashushia watu” ghadhabu Yake. Siku moja, ambapo Mungu atafunua ukweli wote kuwahusu wanadamu, watu watakamilishwa, na Mungu atastarehe. Watu hawatamrarai Mungu tena, na Yeye “Hatawaelimisha” tena. Kuanzia hapo na kuendelea, watu wataweza “kuishi peke yao,” lakini sasa si wakati wa jambo hilo. Bado kuna mengi katika watu yanayoweza kuitwa “bandia”, na raundi kadhaa za uchunguzi zinahitajika, “vituo kadhaa zaidi vya ukaguzi” ambapo “ushuru” unaweza kulipwa vizuri. Ikiwa bado kuna bidhaa bandia, zitatwaliwa ili zisiuzwe, na kisha bechi hilo la bidhaa za magendo litaharibiwa. Je, hii siyo njia nzuri ya kufanya mambo?

Sura ya 19

Katika mawazo ya watu, inaonekana Mungu ni wa fahari sana, naye ni Asiyeeleweka. Ni

kana kwamba Mungu haishi miongoni mwa binadamu na kana kwamba anawadharau watu kwa sababu Yeye ni wa fahari sana. Mungu, hata hivyo, huziseta fikira za watu na kuzifuta zote, Akizizika katika “makaburi” ambamo zinageuka kuwa majivu. Mtazamo wa Mungu kwa fikira za binadamu ni sawa na mtazamo Wake kwa wafu, Akiwafafanua apendavyo. Inaonekana kana kwamba fikira hazina mjibizo; kwa hivyo, Mungu amekuwa akifanya kazi hii tangu uumbaji wa dunia hadi leo, na Hajaacha kamwe. Kwa sababu ya mwili, binadamu hupotoshwa na Shetani, na kwa sababu ya matendo ya Shetani duniani, binadamu huunda kila aina ya fikira katika harakati ya uzoefu wao. Huu unaitwa “muundo asilia.” Hii ndiyo hatua ya mwisho ya kazi ya Mungu duniani, kwa hiyo mbinu ya kazi Yake imefikia kilele chake, naye Anazidisha mafunzo Yake kwa binadamu ili waweze kufanywa wakamilifu katika kazi Yake ya mwisho, hatimaye wakiyaridhisha mapenzi ya Mungu. Awali, kulikuwa tu na kupata nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu miongoni mwa binadamu, lakini hakuna maneno yaliyonenwa na Mungu Mwenyewe. Wakati ambapo Mungu alinena kwa sauti Yake Mwenyewe, kila mmoja alishangazwa, na maneno ya leo ni ya kushangaza zaidi. Maana ya maneno haya ni ngumu kutambua hata zaidi, na binadamu wanaoneka kuwa katika hali ya kuvutiwa sana, kwa sababu asilimia hamsini ya maneno Yake huja katikati ya alama za kudondoa. “Ninapozungumza, watu husikiliza sauti Yangu kwa makini sana; Ninaponyamaza kimya, hata hivyo, wao huanza ‘shughuli’ zao wenyewe.” Kifungu hicho kinajumuisha neno lililo katika alama ya kudondoa. Kadiri Mungu anavyozungumza kwa ucheshi zaidi, jinsi anavyofanya, ndivyo yanavyoweza kuwavutia zaidi watu kuyasoma. Watu wanaweza kukubali kushughulikiwa wakati ambapo wamepumzika. Kimsingi, hata hivyo, hili ni ili kuwazuia watu wengi kuvunjika moyo au kusikitika wakati ambapo hawajaelewa maneno ya Mungu. Hii ni mbinu ya vita vya Mungu dhidi ya Shetani. Ni kwa njia hii tu ndiyo watu watasalia na kuvutiwa na maneno ya Mungu na waendeleo kuyazingatia hata wanaposhindwa kufuata mkondo wa maneno hayo. Hata hivyo, kuna uzuri mwingi katika maneno Yake yote ambayo hayamo katika dondoo, na kwa hiyo yanatambulika zaidi na huwafanya watu kuyapenda maneno ya Mungu hata zaidi na kuhisi utamu wa maneno Yake ndani ya mioyo yao wenyewe. Kwa kuwa maneno ya Mungu huja katika miundo mingi mbalimbali, nayo ni mazuri na tofauti, na kwa kuwa hakuna urudiaji wa majina miongoni mwa maneno mengi ya Mungu, katika hisia yao ya tatu, watu huamini kuwa Mungu ni mpya daima na kamwe si mzee. Kwa mfano: “Siwataki watu wawe ‘wtumiaji’ tu; pia Nawataka wawe ‘wazalishaji’ wanaomshinda Shetani.” Maneno “watumiaji” na “wazalishaji” katika sentensi hiyo yana maana sawa na maneno mengine yaliyonenwa katika nyakati za awali, lakini Mungu si asiyebadilisha mawazo; badala yake, Huwafanya watu wafahamu upya Wake na hivyo kuthamini upendo wa Mungu. Ucheshi katika hotuba ya Mungu una hukumu Yake na madai Yake kwa binadamu. Kwa kuwa maneno yote ya Mungu yana malengo, kwa kuwa yote yana maana, ucheshi Wake haukusudiwa tu kuleta raha katika mazingira au kuwafanya watu waangue

kicheko, wala si kwa ajili kulegeza misuli yao tu. Badala yake, ucheshi wa Mungu unanuiwa kumkomboa binadamu kutoka kwa kifungo cha miaka elfu tano, kamwe asifungwe tena, ili aweze kukubali maneno ya Mungu vizuri zaidi. Mbinu ya Mungu ni kutumia kijiko kimoja cha sukari kusaidia dawa iteremke; Huwa Hamlazimishi watu kumeza dawa chungu. Kuna uchungu ndani ya kilicho tamu, na pia utamu ndani ya kilicho chungu.

“Mwangaza hafifu unapoanza kuonekana Mashariki, watu wote ulimwenguni wanautilia maani zaidi kidogo. Bila kujawa na usingizi, binadamu wanasonga mbele kuchunguza chanzo cha mwangaza huu wa mashariki. Kwa sababu ya uwezo wao finyu, hakuna yeyote ambaye ameweza kuona mahali unapotokea mwangaza.” Hiki kinafanyika kila mahali ulimwenguni, sio tu miongoni mwa wana wa Mungu na watu Wake. Watu katika ulimwengu wa kidini na wasioamini wote huwa na mjibizo huu. Katika wakati ambapo nuru ya Mungu hung’aa, nyoyo zao zote hubadilika polepole, na wao huanza kugundua bila kujua kwamba maisha yao hayana maana, kwamba maisha ya binadamu hayana thamani. Binadamu hawafuatilii siku za baadaye, hawafikirii kuhusu kesho, au kuwa na wasiwasi kuhusu kesho; badala yake, wao hushikilia wazo kwamba wanapaswa kula na kunywa zaidi wakati bado ni “vijana,” na kwamba itakuwa imestahili mara tu siku ya mwisho itakapofika. Binadamu hawana hamu yoyote ya kuuongoza ulimwengu. Nguvu za upendo wa binadamu kwa ulimwengu ziliibwa kikamilifu na “ibilisi,” lakini hakuna ajuaye sababu ni gani. Kile wanachoweza kufanya ni kukimbia tu huku na kule, wakiarifiana, kwa kuwa siku ya Mungu bado haijafika. Siku moja, kila mtu ataona majibu kwa mafumbo yote yasiyoeleweka. Hiki ndicho ambacho Mungu alimaanisha hasa Aliposema, “Binadamu watazinduka kutoka usingizini na ndotoni, na ni hapo tu ndipo wanapotambua pole pole kwamba siku Yangu inawajia.” Wakati huo utakapofika, watu wote ambao ni wa Mungu watakuwa kama majani ya kijani kibichi “yakisubiri kufanya huduma yao Nikiwa duniani.” Watu wengi sana miongoni mwa watu wa Mungu Uchina bado hurudia hali mbaya baada ya Mungu kutamka sauti Yake, na kwa hiyo Mungu asema, “... ilhali, bila uwezo wa kubadilisha ukweli, hawana budi ila kunisubiri Nitoe hukumu.” Bado kutakuwa na wengine miongoni mwao wa kuondolewa—sio wote watabaki bila kubadilishwa. Badala yake, watu wanaweza tu kufikia viwango baada ya kujaribiwa, ambavyo kwavyo wanapewa “vyeti vya ubora”; la sivyo, watakuwa takataka juu ya rundo la takataka. Siku zote Mungu huonyesha hali halisi ya binadamu, kwa hiyo binadamu huendelea kuhisi usiri wa Mungu. “Kama Hangekuwa Mungu, Angewezaje kujua vizuri sana hali yetu halisi?” Hata hivyo, kwa ajili ya udhaifu wa watu, “[k]atika mioyo ya binadamu, Mimi daima si wa juu, wala duni. Kulingana na wao, haijalishi kama Nipo au la.” Je, hii hasa si hali ya watu wote inayolingana vizuri na uhalisi? Kulingana na wanadamu, Mungu yupo wakati ambapo wanamtafuta na hayupo wakati ambapo hawamtafuti. Kwa maneno mengine, Mungu yupo ndani ya mioyo ya binadamu punde tu wanapohitaji msaada

Wake, lakini wakati hawamhitaji, Hayupo tena. Hiki ndicho kiko ndani ya mioyo ya watu. Kwa kweli, kila mtu duniani hufikiria hivi, ikiwemo “wakana Mungu” wote, na “fikira” yao kuhusu Mungu si dhahiri na ya isiyoonekana.

“Kwa hiyo, milima inakuwa mipaka kati ya mataifa ulimwenguni, maji yanakuwa vikwazo vya kuwatenga watu wa nchi tofauti mbali mbali, na hewa inapuliza kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine katika nafasi zilizo juu ya dunia.” Hii ndiyo kazi ambayo Mungu alifanya wakati Alipokuwa Akiuumba ulimwengu. Kulitaja hili hapa kunawakanganya watu: Yawezekana kwamba Mungu anataka kuumba ulimwengu mwingine? Ni haki kusema hivi: Kila wakati Mungu anaponena, maneno Yake huwa na uumbaji, usimamizi, na uharibifu wa ulimwengu; ni kwamba tu wakati mwingine yako dhahiri, na wakati mwingine ni ya dhahania. Usimamizi wote wa Mungu unajumuisha katika maneno Yake; ni kwamba tu wanadamu hawawezi kuyatofautisha. Baraka ambazo Mungu anawapa binadamu huifanya imani yao kukua mara mia moja. Kutoka nje, inaonekana kana kwamba Mungu anafanya ahadi kwao, lakini la muhimu ni kipimo cha matakwa ya Mungu kwa watu wa ufalme Wake. Wale wanaostahili kutumiwa watasalia, ilhali wale wasiotii watamezwa katika janga ambalo litaanguka kutoka mbinguni. “Radi, inayovingirika angani, itawaangusha binadamu; milima ya juu, inapoanguka, itawazika; wanyama pori kwa njaa yao watawala; na bahari, zinapobingirika, zitawagubika. Binadamu wanapojishughulisha na migogoro ya mauaji ya jamii, binadamu wote watatafuta maangamizo yao katika majanga yatokayo katikati yao.” Huku ni “kutendewa kwa njia ya pekee” kutakaotolewa kwa wale ambao hawafikii viwango vinavyohityajika na ambao baadaye hawataokolewa katika ufalme. Kadiri Mungu anavyosema mambo kama, “Hakika, chini ya mwongozo wa mwangaza Wangu, mtapenya katika utawala wa nguvu za giza. Hakika, katikati ya giza, hamtaupoteza mwangaza unaowaongoza,” ndivyo watu wanavyofahamu zaidi heshima yao wenyewe; hivyo, huwa na imani zaidi ya kutafuta maisha mapya. Mungu huwapa wanadamu jinsi wanavyomwomba. Punde Mungu anapowafichua kwa kiasi fulani, Yeye hubadilisha mtindo Wake wa kunena, Akitumia sauti ya kubariki ili kupata matokeo bora kabisa. Kuwawekea binadamu madai kwa njia hii hutoa matokeo zaidi ya kiutendaji. Kwa kuwa watu wote wako radhi kuzungumza kuhusu biashara na wenzi wao—wote ni watalaam katika biashara—hiki ndicho Anacholenga Mungu hasa katika kusema hivi. Kwa hiyo, “Sinimu” ni nini? Hapa, Mungu harejelei ufalme ulio duniani, ambao umepotoshwa na Shetani, badala yake kwakusanyiko la malaika wote waliotoka kwa Mungu. Maneno “simama imara na thabiti” yanadokeza kwamba malaika watapenyeza nguvu zote za Shetani, hiyo Sinimu katika ulimwengu mzima. Hivyo, maana halisi ya Sinimu ni kusanyiko la malaika wote duniani, na hapa inahusu wale walio duniani. Kwa hivyo, ufalme utakaokuwepo baadaye duniani utaitwa “Sinimu,” na sio “ufalme.” Hakuna maana halisi kwa “ufalme” ulio duniani; hususani, ni Sinimu. Hivyo, ni kwa

kuunganisha tu kwa ufafanuzi wa Sinimu ndiyo mtu anaweza kujua maana halisi ya maneno “Hakika mtaonyesha utukufu Wangu katika ulimwengu mzima.” Hili linaonyesha kupangwa katika madaraja kwa watu wote duniani katika siku za baadaye. Watu wote wa Sinim watakuwa wafalme wanaowaongoza watu wote duniani baada ya wao kupitia kuadibu. Kila kitu duniani kitatenda kazi kama kawaida kwa sababu ya usimamizi wa watu wa Sinim. Hiki ni kielelezo cha kukadiria tu hali hiyo. Watu wote watabaki ndani ya ufalme wa Mungu, kumaanisha kwamba wataachwa katika Sinim. Binadamu walio duniani wataweza kuwasiliana na malaika. Hivyo, mbingu na dunia zitaunganishwa; au, kwa maneno mengine, watu wote walio duniani watatii na kumpenda Mungu kama vile malaika mbinguni hufanya. Wakati huo, Mungu ataonekana waziwazi kwa watu wote duniani na Atawaruhusu wauone uso Wake halisi kwa macho yao, na Atajidhihirisha kwao wakati wowote.

Sura ya 20

Mungu aliwaumba wanadamu wote, na amewaongoza wanadamu wote mpaka leo. Hivyo, Mungu anajua yote yafanyikayo miongoni mwa wanadamu: Anajua uchungu ulio ndani ya ulimwengu wa mwanadamu, Anaelewa utamu ulio ndani ya ulimwengu wa mwanadamu, na kwa hiyo kila siku Yeye hufafanua hali za maisha za wanadamu wote, na, zaidi ya hayo, hushughulikia udhaifu na upotovu wa wanadamu wote. Si mapenzi ya Mungu kwamba wanadamu wote watupwe jahanamu, au kwamba wanadamu wote waokolewe. Kila mara huwa kuna kanuni kwa matendo ya Mungu, lakini hakuna anayeweza kuelewa sheria za yote Afanyayo. Watu wanapofahamu uadhama na ghadhabu ya Mungu, Mungu hubadilisha sauti mara moja kuwa ya huruma na upendo, lakini watu wanapokuja kujua huruma na upendo wa Mungu, Anaibadilisha sauti mara moja tena, Akiyafanya maneno Yake kuwa magumu kula kana kwamba ni kuku aliye hai. Katika maneno yote ya Mungu, mwanzo haujawahi kurudiwa kamwe, na maneno Yake yoyote hayajawahi kamwe kuzungumziwa kulingana na kanuni za matamko ya jana; hata sauti haifanani, wala hakuna uhusiano wowote katika maudhui—haya yote huwafanya watu wahisi wamekanganywa hata zaidi. Hii ni hekima ya Mungu, na ufichuzi wa tabia Yake. Yeye hutumia sauti na mtindo wa kunena Kwake kutawanya dhana za watu, ili kumtatiza Shetani, Akimnyang’anya Shetani nafasi ya kutia sumu matendo ya Mungu. Ajabu ya matendo ya Mungu husababisha akili za watu kuachwa zikiwa zimeshtushwa na maneno ya Mungu. Wanaweza kuupata mlango wao wa mbele kwa shida, au hata hawajui wakati wanaotarajiwa kula au kupumzika, hivyo wanatimiza kweli “kuacha kulala na kula ili kutumia rasilimali kwa ajili ya Mungu.” Lakini hata wakati huu, Mungu bado haridhiki na hali za sasa, na kila mara huwa Amemkasirikia mwanadamu, Akimlazimisha kuonyesha moyo wake halisi. La sivyo, watu “wangetii” mara moja na kuwa wazembe, wakionyeshwa huruma kidogo tu na Mungu. Huu ni uduni wa mwanadamu; hawezi kubembelezwa, lakini lazima apigwe au alazimishwe ili asonge.

“Kati ya wale wote Ninaowatazamia, hakuna mtu aliyewahi kunitafuta kwa makusudi na moja kwa moja. Wao wote huja mbele Zangu kwa kushawishiwa na wengine, wakiwafuata watu wengi, na hawana nia ya kulipa gharama au kutumia muda kustawisha maisha yao.” Hivyo ndivyo hali za wote walio duniani zilivyo. Hivyo, bila kazi ya mitume au viongozi, watu wote wangukuwa wametawanyika kitambo sana, na kwa hiyo, kote kote katika enzi, hakuwajakuwa na ukosefu wa mitume na manabii.

Katika matamko haya, Mungu anazingatia kwa hali maalum kufanya muhtasari wa hali za maisha za wanadamu wote. Maneno kama “Maisha ya mwanadamu hayana joto hata kidogo, na hayana dalili yoyote ya binadamu wala mwanga—lakini daima amekuwa mwenye kujishughulisha na mwenyewe, akivumilia maisha yasiyo ya thamani ambayo yeye huenda hapa na pale akiharakisha kufanya mambo bila kufikia kitu chochote. Kwa haraka sana, siku ya kufa inakaribia, na mtu anakufa kifo cha uchungu” yote ni ya aina hii. Ni kwa nini Mungu ameongoza kuishi kwa wanadamu mpaka leo, na bado pia Anafichua utupu wa maisha katika ulimwengu wa mwanadamu? Na kwa nini Anafafanua maisha yote ya watu wote kama “kufika kwa haraka na kuondoka kwa haraka”? Huu, inaweza kusemwa, wote ni mpango wa Mungu, wote umeamuliwa na Mungu, na kwa hivyo, kwa namna moja unaashiria jinsi Mungu anadharau yote isipokuwa maisha katika uungu. Ingawa Mungu aliwaumba wanadamu wote, Hajawahi kamwe kufurahishwa na maisha ya wanadamu wote, na kwa hiyo Yeye huwaruhusu tu wanadamu waishi chini ya upotovu wa Shetani. Baada ya wanadamu kupitia mchakato huu, Atawaangamiza au kuwaokoa wanadamu, na hivyo mwanadamu atatimiza maisha duniani ambayo si matupu. Yote haya ni sehemu ya mpango wa Mungu. Na kwa hiyo, huwa kila mara kuna matamano ndani ya fahamu ya mwanadamu, jambo ambalo limesababisha kutokuwa na mtu anayekufa kifo maasumu kwa furaha—lakini wale ambao tu hutimiza matamano haya ni watu wa siku za mwisho. Leo, bado watu huishi katikati ya utupu usiogeuka na bado wanangoja matamano haya yasiyoonekana: “Ninapoufunika uso Wangu kwa mikono Yangu, na kuwasukuma watu chini ya ardhi, mara moja wao hupungukiwa na pumzi, na ni vigumu waweze kuishi. Wao wote hunililia, wakiwa wenye hofu kwamba Nitawaangamiza, kwa maana wote wanatamani kutazama siku ambayo Nitatukuzwa.” Hivyo ndivyo hali za watu zilivyo leo. Wote huishi katika “ombwe,” bila “oksijeni,” ambalo huwafanya kuwa na ugumu kupumua. Mungu hutumia matamano ndani ya fahamu ya mwanadamu ili kuwasaidia wanadamu wote kuendelea kuishi; la sivyo, wote “wangeondoka nyumbani ili kuwa watawa wa kiume,” kwa sababu hiyo wanadamu wote wangetoweka, na wangemalizika. Hivyo, ni kwa sababu ya ahadi ambayo Mungu alimpa mwanadamu ndio mwanadamu ameendelea kuishi mpaka leo. Huu ni ukweli, lakini mwanadamu hajawahi kugundua sheria hii, na kwa hiyo hajui ni kwa nini yeye “anahofu sana kwamba kifo kitamjia mara ya pili.” Kwa kuwa ni binadamu, hakuna yeyote ambaye ana ujasiri wa kuendelea

kuishi, wala hakuna yeyote ambaye amewahi kuwa na ujasiri wa kufa, na hivyo Mungu asema kwamba watu “hufa kifo cha uchungu.” Hivyo ndivyo hali halisi miongoni mwa wanadamu ilivyo. Labda, katika matarajio yao, watu wengine wamekumbana na vizuizi na wakawaza juu ya kifo, lakini mawazo haya hayajawahi kufaulu; labda, wengine wamewaza juu ya kifo kwa sababu ya ugomvi wa familia, lakini wanawajali wapendwa wao, na wanabaki kutoweza kutimiza matamania yao; na labda, wengine wamewaza juu ya kifo kwa sababu ya mapigo kwa ndoa yao, lakini hawako radhi kupitia hilo. Hivyo, watu hufa wakiwa na majonzi au majuto ya milele ndani ya mioyo yao. Hivyo ndivyo hali mbalimbali za watu wote zilivyo. Nikitazama juu ya ulimwengu mpana wa mwanadamu, watu huja na kwenda katika mkondo usiokuwa na mwisho, na ingawa wanahisi kwamba kungekuwa na raha zaidi kwa kifo ikilinganishwa na kuishi, wao bado huendelea kusema maneno matupu, na kamwe hakuna yeyote ambaye amewahi kuongoza kwa mfano, kwa kufa na kufufuka, na kuwaambia walio hai namna ya kufurahia furaha ya kifo. Watu ni mafidhuli duni: Hawana haya wala kujiheshimu, nao daima hukosa kutimiza ahadi zao. Katika mpango Wake, Mungu alijaalia kikundi cha watu ambao wangepurahia ahadi Zake, na hivyo Mungu asema, “wengi wameishi katika mwili, na wengi wamekufa na wamezaliwa upya duniani. Hata hivyo kamwe hakuna yeyote kati yao aliyepata nafasi ya kufurahia baraka za ufalme leo.” Wote ambao wanafurahia baraka za ufalme leo wamejaaliwa na Mungu tangu Alipouumba ulimwengu. Mungu alipanga ili roho hizi ziishi ndani ya mwili katika siku za mwisho, na hatimaye, Mungu atalipata kundi hili la watu, na kuwapangia kuwa Sinim. Kwa sababu, hususa, roho za watu hawa ni malaika, Mungu asema “Je, Nimetoweka kabisa katika roho ya mwanadamu?” Kwa kweli, watu wanapoishi katika mwili, wanabaki kutojua mambo ya ulimwengu wa kiroho. Kutokana na maneno haya rahisi hali ya moyo wa Mungu “mwanadamu kunipiga macho ya hadhari”—mhemko wa Mungu unaweza kuonekana. Katika maneno haya rahisi, taaluma tata ya Kisaikolojia ya Mungu inaelezeka. Tangu wakati wa uumbaji mpaka leo, ndani ya moyo wa Mungu daima kumekuwa na majonzi yanayoandamana na ghadhabu na hukumu, kwani watu walio duniani hawana uwezo wa kuyajali mapenzi ya Mungu, kama tu asemavyo Mungu, “Mwanadamu ni kama kiumbe katili cha mlimani.” Lakini Mungu asema pia, “Siku itawadia ambapo mwanadamu ataogelea kuja upande Wangu kutoka katikati ya bahari kuu, ili aweze kufurahia mali yote ya dunia na kuacha hatari ya kumezwa na bahari.” Huu ndio ufanikishaji wa mapenzi ya Mungu, na pia unaweza kuelezwa kama mwelekeo usioepukika, na unaashiria ufanikishaji wa kazi ya Mungu.

Ufalme utakaposhuka duniani kabisa, watu wote watapata tena mfano wao wa asili. Hivyo, Mungu asema, “Nafurahia kutoka juu ya kiti Changu cha enzi, Naishi miongoni mwa nyota. Na malaika wananipa nyimbo mpya na dansi mpya. Udhaifu wao hausababishi machozi kutiririka nyusoni mwao tena. Sisikii tena, mbele Yangu, sauti za malaika wakilia, na hakuna tena

anayeninung'unikia kuwa ana shida.” Hili linaonyesha kwamba siku ambayo Mungu atapata utukufu kamili ndiyo siku ambayo mwanadamu atafurahia pumziko lake; watu hawakimbii huku na huko tena kutokana na usumbufu wa Shetani, dunia inaacha kuendelea mbele, na watu wanaishi katika pumziko—kwa kuwa idadi kubwa mno ya nyota angani zinafanywa upya, na jua, mwezi, na nyota, na kadhalika, na milima na mito yote iliyo mbinguni na duniani, vyote vinabadilishwa. Na kwa kuwa mwanadamu amebadilika, na Mungu amebadilika, kwa hiyo, pia, vitu vyote vinabadilika. Hili ndilo lengo la msingi la mpango wa usimamizi wa Mungu, na ule ambao utatimizwa hatimaye. Lengo la Mungu katika kuzungumza maneno haya yote ni hasa kwa mwanadamu kumjua Yeye. Watu hawaelewi amri za utawala za Mungu. Yote ambayo Mungu hufanya yametungwa na kupangwa na Mungu Mwenyewe, na Mungu hayuko radhi kumwacha mtu yeyote aingilie; badala yake, Yeye huwaruhusu watu kuona kwamba yote yamepangwa na Yeye na hayawezi kutimizwa na mwanadamu. Ingawa mwanadamu anaweza kuliona, au kuliona kuwa gumu kuwaza, yote yanadhibitiwa na Mungu pekee, na Mungu hatamani litiwe doa na wazo hata kidogo la mwanadamu. Mungu kwa kweli Hatawasamehe wowote wanaoshiriki, hata kwa kiasi kidogo; Mungu ni Mungu anayemwonea mwanadamu wivu, na inaonekana Roho wa Mungu hasa ni mwepesi wa kuhisi katika suala hili. Hivyo, yeyote aliye na nia hata kidogo ya kuingilia atazongwa mara moja na miale ya moto ya Mungu ya kuangamiza, ikimgeuza kuwa majivu ndani ya moto. Mungu hawaruhusu watu kuonyesha vipaji vyao jinsi wapendavyo, kwani wote walio na vipaji hawana uzima; hivi vipaji vya kudhaniwa humhudumia Mungu tu, na vinatokana na Shetani, na hivyo vinadharauliwa hasa na Mungu, Asiyeruhusu hili. Hata hivyo mara nyingi ni watu wasio na uhai ndio wanaweza kushiriki katika kazi ya Mungu, na, hata zaidi, kushiriki kwao huwa hakugunduliwi, kwani kunafichwa na vipaji vyao. Kotekote katika enzi, wale ambao wana vipawa hawajawahi kusimama imara, kwani hawana uzima, na hivyo wanakosa nguvu zozote za kupinga. Hivyo, Mungu asema, “Kama Sizungumzi waziwazi, mwanadamu kamwe hataacha kufanya upumbavu kamwe, na ataanguka katika kuadibu Kwangu bila kujua—kwa kuwa mwanadamu hanijui katika nafsi ya mwili Wangu.” Wote ambao ni wa mwili na damu wanaongozwa na Mungu, lakini pia wanaishia katika kifungo cha Shetani, na kwa hiyo watu hawajawahi kuwa na uhusiano wa kawaida kati yao, kama ni kwa sababu ya tamaa, au kuabudu, au utaratibu wa mazingira yao. Mahusiano yasiyo ya kawaida kama hayo ndiyo Mungu anayachukua zaidi ya yote, na hivyo ni kwa sababu ya mahusiano kama hayo ndiyo maneno kama “Kile Ninachotaka ni viumbe vilivyo hai ambao wamejawa na uzima, si maiti ambazo zimegubika katika kifo. Kwa kuwa Ninaketi mezani pa ufalme, Nitatoa amri kwa watu wote duniani ili wapate ukaguzi Wangu” yanatoka kinywani mwa Mungu. Mungu anapokuwa juu ya ulimwengu mzima, kila siku Yeye huangalia kwa makini kila kitendo cha wale wa mwili na damu, na Hajawahi kumpuuza hata mmoja wao. Haya ni matendo ya Mungu. Na kwa hiyo, Nawasihi watu wote wachunguze fikira, mawazo, na matendo yao wenyewe.

Siwataki muwe ishara ya aibu kwa Mungu, bali dhihirisho la utukufu wa Mungu, kwamba katika matendo, maneno, na maisha yenu yote, msiwe shabaha ya mizaha ya Shetani Haya ni matakwa ya Mungu kwa watu wote.

Sura ya 21

Machoni pa Mungu, watu ni kama wanyama katika ulimwengu wa wanyama. Wao hupigana, huchinjana, na huwa na ushirikiano wa pekee mmoja kwa mwingine. Machoni pa Mungu, wao pia ni kama sokwe, wakipangiana hila bila kujali umri au jinsia. Kwa hivyo, yote ambayo wanadamu wote hufanya na kuonyesha hayajawahi kuupendeza moyo wa Mungu. Wakati ambao Mungu hufunika uso Wake ndio hasa wakati ambao watu duniani kote wanajaribiwa. Watu wote wanapiga kite kwa uchungu, wote wanaishi chini ya tishio la msiba, na hakuna hata mmoja wao aliyewahi kuepuka kutoka kwa hukumu ya Mungu. Kwa kweli, lengo kuu la Mungu kupata mwili ni kumhukumu mwanadamu na kumshutumu katika mwili Wake. Katika mawazo ya Mungu, imeamuliwa kitambo ni nani, kwa mujibu wa kiini chake, ataokolewa au kuangamizwa, na hili litafanywa wazi polepole wakati wa awamu ya mwisho. Kadri siku na miezi inavyopita, watu hubadilika na umbo lao la asili hufichuliwa. Inakuwa wazi iwapo kuna kuku au bata katika yai wakati linapofunguka. Wakati ambapo yai huvunjika ndio wakati hasa ambapo maafa duniani yatafikia kikomo. Kutokana na hili inaweza kuonekana kuwa, ili kujua kama kuna “kuku” au “bata” ndani, lazima “yai” livunjwe. Huu ndio mpango katika moyo wa Mungu, na ni lazima utimizwe.

“Ole wao, maskini wanadamu! Kwa nini mwanadamu ananipenda lakini hawezi kufuata nia za Roho Wangu?” Kwa sababu ya hali hii ya mwanadamu, lazima apatie kushughulikiwa ili apate kuridhisha mapenzi ya Mungu. Na kwa sababu ya Mungu kuwachukia sana wanadamu, Ametangaza mara nyingi: “Enyi waasi wa wanadamu wote! Lazima waharibiwe chini ya miguu Yangu, ni lazima watokomee kabisa katikati ya kuadibu Kwangu, na lazima, siku ambayo mpango Wangu mkubwa utakamilika, watatupiliwa mbali kutoka kati ya wanadamu, ili wanadamu wote wazijue nyuso zao mbaya.” Mungu ananena kwa watu wote katika mwili, na pia Ananena kwa Shetani katika ulimwengu wa kiroho, yaani, juu ya ulimwengu wote. Haya ni mapenzi ya Mungu, na ndiyo yanayohitajika kutimizwa kwa mpango wa Mungu wa miaka 6,000.

Kwa kweli, Mungu ni wa kawaida hasa, na kuna mambo mengine ambayo yanaweza tu kutimizwa ikiwa Atayatekeleza mwenyewe na kuyaona kwa macho Yake Mwenyewe. Sivyo kama watu wanavyofikiria, Mungu hulala tu pale huku yote yanaenda kama Atakavyo; haya ni matokeo ya usumbufu wa Shetani katika watu, jambo ambalo huwafanya watu kutofahamu uso halisi wa Mungu. Kwa hivyo, wakati wa enzi ya mwisho, Mungu amepata mwili ili kufichua

wazi uhalisi Wake kwa mtu, bila kuficha chochote. Maelezo mengine ya tabia ya Mungu ni kutia chumvi kutupu, kama vile inaposemwa kwamba Mungu anaweza kuiharibu dunia kwa neno moja au wazo dogo. Kwa hiyo, watu wengi husema mambo kama, Kwa nini Mungu ni Mwenye kudura, lakini Hawezi kummeza Shetani kwa fundu moja? Maneno haya ni ya upuuzi, na huonyesha kuwa watu bado hawamjui Mungu. Kwa Mungu kuwaangamiza maadui Zake kunahitaji mchakato, hata hivyo ni kweli kusema kwamba Mungu ni Mshindi kwa yote: Hatimaye Mungu atawashinda maadui Zake. Kama vile tu nchi yenye nguvu huishinda nchi dhaifu, ni lazima itimize ushindi yenyewe, hatua kwa hatua, wakati mwingine kwa kutumia nguvu, wakati mwingine kwa kutumia mkakati. Kuna mchakato, lakini haiwezi kusema kuwa, kwa kuwa nchi yenye nguvu ina silaha za nyuklia za kizazi kipya na nchi dhaifu ni duni sana, nchi dhaifu itakata tamaa bila kupigana. Hiyo ni hoja ya upuuzi. Ni haki kusema kwamba nchi yenye nguvu itashinda bila shaka na nchi dhaifu itapoteza bila shaka, lakini nchi yenye nguvu inaweza tu kusemwa kuwa na nguvu zaidi wakati inapovamia binafsi nchi dhaifu. Hivyo, daima Mungu amesema kwamba mwanadamu hamjui. Kwa hiyo, kile kilichosemwa hapo juu ni upande mmoja wa kwa nini mwanadamu hamjui Mungu? Je, hizi ni dhana za mwanadamu? Kwa nini Mungu anataka tu mwanadamu ajue uhalisi Wake, na mwenyewe na hivyo kuwa mwili? Hivyo, watu wengi waliabudu Mbinguni kwa dhiti, lakini “Mbingu haijawahi kuathiriwa na matendo ya mwanadamu hata kidogo, na iwapo kumtendea Kwangu mwanadamu kungetegemea matendo yake yote, basi wanadamu wote wangeishi katikati ya kuadibu Kwangu.”

Mungu hutambua kiini cha mwanadamu. Katika matamko ya Mungu, Mungu anaonekana “kuteswa” sana na mwanadamu kiasi kwamba Hana haja ya kumzingatia zaidi mwanadamu, wala tumaini ndani yake hata kidogo; ingeonekana kwamba mwanadamu hawezi kuokolewa. “Nimewaona watu wengi wakitiririka na machozi, na Nimewaona watu wengi wakitoa nyoyo zao ili wapate utajiri Wangu. Licha ya ‘uchaji Mungu’ kama huu, Sijawahi kujitoa kwa mwanadamu kikamilifu kwa sababu ya hisia zake za ghafla, kwa sababu mwanadamu hajawahi kuwa radhi kujitoa kwa furaha mbele Yangu.” Mungu anapofichua asili ya mwanadamu, mwanadamu anaona aibu, lakini huu ni ufahamu wa juujuu tu, na hawezi kujua kweli asili yake katika maneno ya Mungu; hivyo, watu wengi hawaelewi mapenzi ya Mungu, hawawezi kupata njia kwa ajili ya maisha yao katika maneno ya Mungu, na kwa hiyo, kadri wanavyokuwa wapumbavu, ndivyo Mungu anavyowadhihaki zaidi. Kwa hivyo, wao huingia katika jukumu la mwovu kwa kutojua—na kwa hiyo, wanakuja kujijua wanapochomwa kwa “upanga mwepesi.” Maneno ya Mungu yanaonekana kuyasifu matendo ya mwanadamu, na kuyahimiza matendo ya mwanadamu—na bado watu daima huhisi kwamba Mungu anawadhihaki. Na hivyo, wanapoyasoma maneno ya Mungu, misuli katika nyuso zao hutetemeka mara kwa mara, kama kwamba wanasukasuka. Huu ni uchafu wa dhamiri zao, na ni kwa sababu hii ndio wanatetemeka

pasipo kutaka. Maumivu yao ni aina ambayo kwayo wanataka kucheka lakini hawawezi—wala hawawezi kulia, kwa sababu utani wa watu unachezwa kwenye kidhibiti cha mbali cha “mashine ya video” “VCR,” lakini hawawezi kuizima, na wanaweza tu kuivumilia. Ijapokuwa “kuzingatia maneno ya Mungu” huhubiriwa wakati wa mikutano yote ya wafanyikazi wenza, ni nani asiyejua asili ya mayai ya joka kubwa jekundu? Ana kwa ana, wao ni watiifu kama wanakondoo, lakini wanapogeuka wao ni katili kama mbwa mwitu, ambalo linaweza kuonekana katika maneno ya Mungu kwamba “watu wengi hunipenda kwa dhati Ninapotoa maneno Yangu, lakini hawathamini maneno Yangu katika roho zao, badala yake wakiyatumia kwa kawaida kama mali ya umma na kuyatupa yalipotoka wakati wowote wanapotaka.” Kwa nini Mungu daima amemfunua mwanadamu? Hili linaonyesha kwamba asili ya mwanadamu ya kale ni thabiti na imara. Kama Mlima wa Tai, ni mrefu kwa mamia ya mamilioni ya mioyo ya watu, lakini siku itakuja ambapo Yu Gong atauhamisha mlima huo, na huu ndio mpango wa Mungu. Katika matamko Yake, hakuna wakati ambapo Mungu hatoi matakwa kwa mwanadamu, kumwonya mwanadamu, au kuonyesha asili ya mwanadamu inayofichuliwa katika maisha yake: “Wakati mwanadamu yuko mbali nami, na wakati ananijaribu, Mimi hujificha kutoka kwake kati ya mawingu. Na hivyo, hawezi kunipata hata kidogo, na huishi tu mikononi mwa waovu, akifanya yote watakayo.” Kwa kweli, watu huwa na nafasi ya kuishi mbele ya uwepo wa Mungu kwa nadra sana, kwa sababu wana hamu kidogo sana ya kutafuta; kwa hiyo, ingawa watu wengi wanampenda Mungu, wanaishi chini ya mkono wa yule mwovu, wanaongozwa tu na yule mwovu. Kama kweli watu wangeishi katika nuru ya Mungu, wakimtafuta Mungu kila dakika ya kila siku, hakungekuwa na haja ya Mungu kunena hivi, ndiyo? Watu wanapoweka maandiko kando, papo hapo wanamweka Mungu kando pamoja na kitabu, na hivyo wanajihusisha na shughuli yao wenyewe, baada ya hapo Mungu hutoweka mioyoni mwao. Lakini wanapokichukua kitabu tena, huwajia ghafla kwamba hawakuwa wakimfikiria Mungu. Hivyo ndivyo maisha ya mwanadamu yalivyo “bila kumbukumbu.” Kadri Mungu anavyonena, ndivyo maneno Yake yanavyokuwa makuu zaidi. Yanapofikia kilele chake, kazi yote inakamilika, na kwa hiyo, Mungu hukomesha matamshi Yake. Kanuni ambayo kwayo Mungu hufanya kazi ni kumaliza kazi Yake wakati inapofikia upeo wake; Haendelei kufanya kazi wakati inapofika upeo wake, lakini Huacha ghafla. Yeye kamwe Hafanyi kazi ambayo si ya lazima.

Sura ya 22 na 23

Leo, wote wako tayari kuelewa mapenzi ya Mungu na kujua tabia ya Mungu, lakini hakuna anayejua kwa nini hawezi kufuata matamano yake, hajui kwa nini moyo wake daima humsaliti, na kwa nini hawezi kutimiza kile anachotaka. Kwa hiyo, yeye anakabiliwa tena na hali mbaya ya kukata tamaa, lakini pia anaogopa. Asiweze kuonyesha hisia hizi zinazopingana, anaweza tu kuonyesha huzuni na kuendelea kujiuliza: Je, inaweza kuwa Mungu hajanipa nuru? Inaweza

kuwa Mungu ameniacha kwa siri? Pengine wengine wote wako sawa, na Mungu amewapa wote nuru isipokuwa mimi. Kwa nini daima mimi husikia kusumbuliwa wakati ninasoma maneno ya Mungu, kwa nini siwezi kuelewa chochote? Ingawa akili za watu hufikiri mambo haya, hakuna mtu anayethubutu kuyaonyesha; wao huendelea tu kupambana kwa ndani. Kwa kweli, hakuna mtu ila Mungu anayeweza kuelewa maneno Yake au kufahamu mapenzi Yake ya kweli. Hata hivyo daima Mungu huwataka watu waweze kufahamu mapenzi Yake—je, huku si kama kujaribu kumpeleka bata kwenye kitulio cha ndege? Je, Mungu hajui kasoro za mwanadamu? Haya ndiyo makutano ya kazi ya Mungu, ni kile ambacho watu hawaelewi, na hivyo Mungu anasema, “Mwanadamu anaishi katikati ya mwanga, ilhali hana habari kuhusu thamani ya mwanga huo. Hana ufahamu kuhusu kiini cha mwanga huo, na chanzo cha mwanga huo, na, zaidi ya hayo, hajui mmiliki wake ni nani.” Kulingana na maneno ya Mungu na kile Anachotaka kutoka kwa mwanadamu, hakuna mtu atakayeokoka, kwa maana hakuna chochote katika mwili wa mwanadamu kinachoyakubali maneno ya Mungu, kwa hiyo kama watu wanaweza kutii maneno ya Mungu, kutunza kwa upendo na kutamani sana maneno ya Mungu, na kutumia maneno hayo katika matamshi ya Mungu yanayoonyesha hali za binadamu kwa hali zao wenyewe, na hivyo kujijua, basi hiki ndicho kiwango cha juu zaidi. Wakati ufalme utafanikishwa hatimaye, mwanadamu anayeishi katika mwili bado atakuwa hawezi kufahamu mapenzi ya Mungu, na bado watahitaji uongozi wa Mungu Mwenyewe. Ni kwamba tu watu hawataingiliwa na Shetani, na watakuwa na maisha ya kawaida ya mwanadamu, ambalo ni lengo la Mungu katika kumshinda Shetani, na hasa ni kwa ajili ya kupata tena kiini cha asili cha mwanadamu, aliyeumbwa na Mungu. Katika mawazo ya Mungu, “mwili” unahusu mambo yafuatayo: kutoweza kujua asili ya Mungu, kutoweza kuona mambo ya ufalme wa kiroho, na, zaidi ya hayo, uwezo wa kupotoshwa na Shetani lakini pia kuelekezwa na Roho wa Mungu. Hiki ni kiini cha mwili uliombwa na Mungu. Kwa kawaida, pia ni ili kuepuka machafuko yanayosababishwa na ukosefu wa utaratibu katika maisha ya wanadamu. Mungu anavyozidi kunena, na maneno Yake yanavyozidi kuwa makali, ndivyo watu huyaelewa maneno Yake zaidi. Watu hubadilika bila kujua, na wanaishi katika nuru bila kujua, na hivyo “Kwa sababu ya nuru, watu wote wanakua, na wameliacha giza.” Haya ndiyo mandhari mazuri ya ufalme, nayo ni kama kile kilichozungumziwa mara nyingi hapo zamani: “kuishi katika nuru, kuondoka kwa kifo.” Wakati Sinim inapofanikishwa duniani—wakati ufalme unapofanikishwa—hakutakuwa na vita tena duniani, hakutakuwa tena na njaa, tauni, na matetemeko ya ardhi; watu wataacha kutengeneza silaha za uharibifu, wote wataishi kwa amani na utulivu; na kutakuwa na shughuli za kawaida kati ya watu, na shughuli za kawaida kati ya mataifa. Hata hivyo wakati uliopo haulinganishwi na hili. Yote chini ya mbingu yako katika machafuko, mapinduzi yanaanza hatua kwa hatua katika kila nchi. Mungu anapotamka sauti Yake watu wanabadilika hatua kwa hatua, na, kwa ndani, kila nchi inaharibika polepole. Misingi imara ya Babiloni inaanza kutetemeka, kama kasri

kwenye mchanga, na makusudi ya Mungu yanavyobadilika, mabadiliko makubwa yanatokea ulimwenguni bila kutambuliwa, na kila aina ya ishara zinaonekana wakati wowote, zikiwaonyesha watu kuwa siku ya mwisho ya dunia imewadia! Huu ni mpango wa Mungu, hizi ni hatua ambazo kwazo Yeye anafanya kazi, na hakika kila nchi itapasuka vipande vipande, Sodoma ya kale itaangamizwa mara ya pili, na hivyo Mungu anasema “Dunia inaanguka! Babeli imelemaa!” Hakuna mtu ila Mungu Mwenyewe anayeweza kufahamu jambo hili kabisa; kuna, hata hivyo, kikomo kwa ufahamu wa watu. Kwa mfano, mawaziri wa masuala ya ndani wanaweza kujua kwamba hali za sasa si imara na kuna machafuko, lakini hawawezi kuzishughulikia. Wanaweza tu kuvumilia, wakitaraji mioyoni mwao siku ambayo wanaweza kuwa na ujasiri, wakitamani kwamba siku itakuja wakati jua litachomoza tena upande wa mashariki, likiangaza kutoka upande mmoja hadi upande mwingine wa nchi na kugeuza hali hii ya kusikitisha ya mambo. Hawajui hata kidogo, hata hivyo, kwamba wakati jua linapochomoza kwa mara ya pili, kutoka kwa jua sio kwa ajili ya kurejesha utaratibu wa kale—huu ni ufufuo, mabadiliko. Huo ndio mpango wa Mungu kwa ulimwengu wote. Yeye atasababisha ulimwengu mpya, lakini zaidi ya yote, Atamfanya mwanadamu upya kwanza. Leo, kuwaleta watu katika maneno ya Mungu ndilo lililo muhimu, sio tu kuwakubalia kufurahia baraka za hadhi. Zaidi ya hayo, kama Mungu anavyosema, “Katika ufalme, Mimi ni Mfalme—lakini badala ya kunichukulia kama Mfalme, mwanadamu ananichukulia kama Mwokozi aliyeshuka kutoka mbinguni. Kwa sababu hii, anasubiri kwa hamu Nimpe sadaka, na hafuatilii ufahamu Wangu.” Hizo ni hali halisi za watu wote. Leo, jambo muhimu ni kuondoa kabisa ulafi wa mwanadamu, hivyo kuwapa watu fursa ya kumjua Mungu bila kuomba chochote; si ajabu, basi, kwamba Mungu anasema, “Wengi sana wamelia mbele Zangu kama waombaji; wengi pia wamenifungulia ‘mifuko’ yao na kunisihi Niwape chakula ili waendeleo kuishi.” Hizi hali mbalimbali zinaonyesha ulafi wa watu, na huonyesha kwamba watu hawampendi Mungu lakini humdai Mungu, au labda hujaribu kupata vitu wanavyotamani sana. Watu wana asili ya mbwa mwitu mwenye njaa, wote ni wajanja na walafi, na hivyo Mungu hutoa mahitaji kwao mara kwa mara, Akiwalazimisha kutoa ulafi katika nyoyo zao na kumpenda Mungu kwa uaminifu. Kwa kweli, hadi leo, bado watu hawajampa Mungu mioyo yao yote, hawajakata shauri bado, wakati mwingine wakijitegemea, wakati mwingine wakimtegemea Mungu bila kumwamini Mungu kabisa. Wakati kazi ya Mungu inapofikia hatua fulani, watu wote wataishi katikati ya upendo na imani ya kweli, na mapenzi ya Mungu yatatimizwa; hivyo, mahitaji ya Mungu sio makubwa.

Malaika daima huenda miongoni mwa wana na watu wa Mungu, wakiharakisha kati ya mbingu na dunia na kushuka kwa ulimwengu wa binadamu baada ya kurejea kwa ulimwengu wa kiroho kila siku. Huu ni wajibu wao, na hivyo kila siku wana na watu wa Mungu huchungwa, na maisha yao hubadilika hatua kwa hatua. Siku ambayo Mungu atabadilisha umbo Lake, kazi ya

malaika duniani itakamilika rasmi na watarudi kwenye ulimwengu wa mbinguni. Leo, wana na watu wa Mungu wote wako katika hali sawa. Kadri sekunde zinavyopita, watu wote wanabadilika, na wana na watu wa Mungu wanakomaa zaidi hatua kwa hatua. Kwa ulinganishi, waasi wote pia wanabadilika mbele ya joka kubwa jekundu: Watu si watiifu tena kwa joka kubwa jekundu, na pepo hawafuati tena mipango yake. Badala yake vitu vyote “vinatenda kama vinavyoona kuwa bora, vikichukua njia inayovifaa zaidi.” Hivyo wakati Mungu anasema, “Je, mataifa ya ulimwengu yatakosaje kuangamia? Mataifa ya ulimwengu yatakosaje kuanguka?” Mbingu zinaanguka kwa kishindo na kwa haraka.... Ni kama kwamba kuna hisia ya kuogofya inayoashiria mwisho wa wanadamu. Ishara mbalimbali za kuogofya zilizotabiriwa hapa hasa ndilo linalotendeka katika nchi ya joka kubwa jekundu, na hakuna hata mmoja kati ya walio duniani anaweza kuepuka. Hilo ndilo linalotabiriwa katika maneno ya Mungu. Katika jakamoyo za watu leo, wanahisi kuwa muda ni mfupi, na wanaonekana kuhisi kuwa msiba unakaribia kuwafika—lakini hawana njia ya kutoroka, na hivyo wote hawana matumaini. Mungu anasema, “Ninapokipamba ‘chumba cha ndani’ cha ufalme Wangu siku baada ya siku, hakuna yule ameingia katika ‘chumba Changu cha kazi’ kwa ghafla ili kuvuruga kazi Yangu.” Kwa kweli, maana ya maneno ya Mungu hayajajikita tu katika kuwafanya watu wamjue Mungu katika maneno Yake. Zaidi ya yote, yanaonyesha kuwa kila siku Mungu hupanga kila aina ya maendeleo kote kote ulimwenguni ili kutumikia sehemu inayofuata ya kazi Yake. Madhumuni ya Yeye kusema “Hakuna yule ameingia katika ‘chumba Changu cha kazi’ kwa ghafla ili kuvuruga kazi Yangu.” ni kwa sababu Mungu hufanya kazi katika uungu, na ingawa watu wanaweza kutaka, hawawezi kushiriki katika kazi Yake. Ningependa kuuliza: Je, unaweza kuyapanga maendeleo yote ya ulimwengu wote? Je, unaweza kuwafanya watu wa dunia kuwakataa mababu zao? Je, unaweza kuwashawishi watu ulimwenguni kote wayatumikie mapenzi ya Mungu? Je, unaweza kumfanya Shetani afanye fujo? Unaweza kuwafanya watu wahisi kwamba dunia ni yenye ukiwa na tupu? Watu hawawezi kufanya mambo kama haya. Zamani, wakati “ujuzi” wa Shetani ulipokuwa bado haujajitokeza kwa ukamilifu, kila mara Shetani angeingilia kila hatua ya kazi ya Mungu; katika hatua hii, Shetani ameishiwa na hila, na hivyo Mungu humruhusu Shetani kuonyesha tabia yake ya kweli ili watu wote waweze kumjua. Huu ndio ukweli wa maneno “Hakuna mtu aliyewahi kuivuruga kazi Yangu.”

Kila siku, watu wa makanisa husoma maneno ya Mungu, kila siku wao huchanguliwa kwenye “meza ya upasuaji.” Kwa mfano, maneno ya dhuhaka kama vile “kupoteza nafasi zao” “kufukuzwa,” “hofu yao kutoweka na hali tulivu kurejea.” “kutelekeza,” kutokuwa na “hisia” na kadhalika huwaacha wakiwa wamenyamaa kwa kuaibika; ni kama kwamba hakuna sehemu ya mwili wao wote—kutoka kichwani hadi wayoni, kutoka ndani hadi nje—inakubaliwa na Mungu. Kwa nini maneno ya Mungu huvua maisha ya watu kuwa wazi hivyo? Je, Mungu anafanya

mambo kuwa magumu kwa watu kwa makusudi? Ni kama kwamba nyuso za watu wote zimepakwa matope ambayo hayawezi kuoshwa. Wakiwa wameinamisha vichwa vyao, kila siku wao hutoa maelezo ya dhambi zao kama kwamba ni wasanii wa kashfa. Watu wamepotoshwa na Shetani kiasi kwamba hawana ufahamu kamili wa hali zao ya kweli. Lakini kwa Mungu, sumu ya Shetani iko katika kila sehemu ya miili yao, hata katika uboho wa mifupa yao; kwa hiyo, kadri ufunuo wa Mungu ulivyo mkubwa, ndivyo watu wanavyozidi kuwa na hofu. Hivyo, watu wote wanaweza kumjua Shetani na kumwona Shetani ndani ya mwanadamu, kwa kuwa hawajaweza kumwona Shetani kwa macho yao. Na kwa kuwa yote yameingia katika uhalisi, Mungu anafunua asili ya mwanadamu—ambalo ni kusema, Anaifunua sura ya Shetani—na hivyo Anamruhusu mwanadamu kumwona Shetani aliye wa kweli na dhahiri, ambalo linaweza kuwasaidia kumjua Mungu wa vitendo vizuri zaidi. Mungu humruhusu mwanadamu kumjua Yeye katika mwili, na humpa umbo Shetani, hivyo Anamruhusu mwanadamu kumjua Shetani aliye wa kweli na dhahiri katika mwili wa watu wote. Hali hizi tofauti ambazo zimezungumziwa ni maelezo ya matendo ya Shetani. Na kwa hiyo, ni haki kusema kwamba wote ambao ni wa mwili ni mfano halisi wa umbo la Shetani. Kwa sababu Mungu halingani na adui Zake, kwa sababu wao wanachukiana, nao ni majeshi mawili tofauti, pepo ni pepo, Mungu ni Mungu, wao hawalingani kama moto na maji, na daima wametengana kama mbingu na dunia. Wakati Mungu alimuumba mwanadamu, aina moja ya watu walikuwa roho za malaika; aina moja haikuwa na roho, hivyo walimilikiwa na roho za pepo, na hivyo wanaitwa pepo. Hatimaye, malaika ni malaika, pepo ni pepo—na Mungu ni Mungu. Hii ndiyo maana ya kila mmoja kuainishwa kulingana na aina, na kwa hiyo wakati malaika wanatawala duniani na kufurahia baraka, Mungu anarudi kwenye makao Yake, na wengine—maadui wa Mungu—wanageuzwa kuwa majivu. Kwa kweli, kwa nje watu wote wanampenda Mungu—lakini asili yake iko katika kiini chao; ni vipi ambavyo wale walio na asili ya malaika wanaweza kuepuka mkono wa Mungu na kuanguka kuzimu? Na ni vipi ambavyo wale walio na asili ya pepo wanaweza kumpenda Mungu kweli? Kwa kweli, watu hawa hawampendi Mungu kweli, kwa hiyo wangewezaje kuwa na nafasi ya kuingia katika ufalme? Yote yalipangwa na Mungu tangu kuumbwa kwa ulimwengu, kama vile Mungu anavyosema, “Mimi naendelea kati ya upepo na mvua, na nimeishi mwaka baada ya mwingine miongoni mwa wanadamu, na hiyo inafuatwa na wakati wa sasa. Je, hizi sio hatua za mpango Wangu wa usimamizi? Ni nani amewahi kuongeza chochote katika mpango Wangu? Ni nani anaweza kuepuka hatua katika mpango Wangu?” Baada ya kuwa mwili, lazima Mungu apitie maisha ya mwanadamu, na je, huu sio upande wa kweli wa Mungu wa vitendo? Mungu hafichi chochote kutoka kwa mwanadamu kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu; badala yake, Yeye huuweka wazi ukweli kwa mwanadamu, kama vile Mungu anavyosema, “Nimekaa mwaka baada ya mwaka kati ya wanadamu.” Ni kwa sababu Mungu ni Mungu aliyepata mwili ndio Amapitia mwaka baada ya mwaka duniani; kwa hiyo, baada ya kupitia tu michakato ya aina zote

ndio Anaweza kuchukuliwa kuwa Amepata mwili, baada ya hapo tu ndio Anaweza kufanya kazi katika uungu ndani ya mwili. Na kisha, baada ya kufichua siri zote tu ndio Atabadilisha umbo Lake. Haya ni maelezo ya mpokezani ya “kutokuwa wa miujiza,” na yanafunzwa moja kwa moja na Mungu.

Lazima watu wapite mtihani wa kila neno la maneno ya Mungu, bila uzembe—hili ni agizo la Mungu!

Sura ya 24 na 25

Bila kusoma kwa makini, haiwezekani kugundua kitu chochote katika matamko ya siku hizi mbili; kwa kweli, yangepaswa kunenwa kwa siku moja, lakini Mungu aliyagawanya kwa siku mbili. Hiyo ni kusema, matamko ya siku hizi mbili yanaunda moja kamili, lakini ili iwe rahisi kwa watu kuyakubali, Mungu aliyagawanya kwa siku mbili ili kuwapa watu nafasi ya kupumua. Hiyo ndiyo fikira ya Mungu kwa mwanadamu. Katika kazi yote ya Mungu, watu wote hutekeleza kazi zao na wajibu wao mahali pao wenyewe. Sio tu watu wenye roho ya malaika ambao hushirikiana; wale walio na roho ya pepo mbaya pia “hushirikiana,” kama vile roho zote za Shetani. Katika matamko ya Mungu huonekana mapenzi ya Mungu na matakwa Yake kwa mwanadamu. Maneno “Kuadibu kwangu kunawajia watu wote, lakini pia kunakaa mbali na watu wote. Maisha yote ya kila mtu yamejaa upendo na pia chuki Kwangu” yanaonyesha kwamba Mungu hutumia kuadibu ili kuwatisha watu wote, Akiwasababisha wapate ufahamu kumhusu Yeye. Kwa sababu ya upotovu wa Shetani na udhaifu wa malaika, Mungu hutumia maneno tu, na sio amri za utawala, kuwadibu watu. Tangu wakati wa uumbaji hadi leo, hii imekuwa kanuni ya kazi ya Mungu kuhusu malaika na watu wote. Kwa sababu malaika ni wa Mungu, bila shaka siku moja watakuwa watu wa ufalme wa Mungu, nao watatunzwa na kulindwa na Mungu. Wengine wote, wakati huo, pia wataainishwa kulingana na aina, aina zote mbalimbali za pepo wabaya wa Shetani wataadibiwa, na wote ambao hawana mapepo wataongozwa na wana na watu wa Mungu. Huo ndio mpango wa Mungu. Hivyo, Mungu Alisema wakati mmoja “Je, wakati wa kufika kwa siku Yangu ni wakati wa kufa kwa mwanadamu kweli? Je, hakika Ningeweza kumwangamiza mwanadamu wakati ufalme Wangu utatengenezwa?” Ingawa haya ni maswali mawili rahisi, ni mipango ya Mungu kwa ajili ya hatima ya wanadamu wote. Mungu atakapofika ndio wakati ambao “watu katika ulimwengu wote watasulubiwa msalabani vichwa vikiangalia chini.” Hili ndilo lengo ambalo Mungu anaonekana kwa watu wote, Akitumia kuadibu ili kuwajulisha kuwepo kwa Mungu. Kwa kuwa wakati ambao Mungu anashuka duniani ni hatua ya mwisho, na wakati ambao nchi zilizo duniani ziko katika ghasia kubwa mno, hivyo Mungu anasema “Nikija chini duniani, giza limetanda na mwanadamu ‘amelala fofofu.’” Kwa hivyo, leo kuna watu wachache tu ambao wana uwezo wa kumjua Mungu mwenye mwili, takriban hakuna

hata mmoja. Kwa kuwa sasa ni enzi ya mwisho, hakuna yeyote aliyewahi kumjua Mungu wa vitendo kwa kweli, na watu wana ufahamu wa juujuu tu kuhusu Mungu. Na ni kwa sababu ya hii ndio watu wanaishi kati ya usafishaji mchungu. Watu wanapoacha usafishaji ndipo pia wanapoanza kuadibiwa, ndio wakati ambapo Mungu anaonekana kwa watu wote ili waweze kumwona wenyewe. Kwa sababu ya Mungu mwenye mwili, watu huingia katika maafa, nao hawawezi kujinasua—ambayo ni adhabu ya Mungu kwa joka kubwa jekundu, na amri Yake ya utawala. Wakati joto la majira ya kuchipua limekuja na maua kuchanua, wakati vyote chini ya mbingu ni kijani kibichi na vitu vyote duniani viko mahali pake, watu na vitu vyote vitaingia hatua kwa hatua katika kuadibu kwa Mungu, na wakati huo kazi yote ya Mungu duniani itaisha. Mungu hatafanya kazi tena au kuishi duniani, kwa maana kazi kubwa ya Mungu itakuwaimetimizwa. Je, watu hawawezi kuweka kando miili yao kwa muda huu mfupi? Mambo gani yanaweza kuunganisha upendo kati ya mwanadamu na Mungu? Ni nani anayeweza kutenganisha upendo kati ya mwanadamu na Mungu? Je, ni wazazi, waume, dada, wake, au usafishaji mchungu? Je, hisia za dhamiri zinaweza kufuta sura ya Mungu ndani ya mwanadamu? Je, kuwa na deni kwa watu na vitendo vyao baina yao kumesababishwa na wao wenyewe? Je, wanaweza kuponywa na mwanadamu? Ni nani anayeweza kujilinda? Watu wanaweza kujikimu? Ni nani wenye nguvu maishani? Ni nani anayeweza kuniacha na kuishi peke yake? Mara kwa mara, kwa nini Mungu anawataka watu wote watekeleze kazi ya kutafakari? Kwa nini Mungu anasema, “Ugumu wa nani umepangwa kwa mikono yao wenyewe?”

Kwa sasa, kuna usiku wa giza kote kote ulimwenguni, na watu hawajali nao ni wapumbavu, lakini akrabu za saa daima hupiga kuendelea mbele, dakika na sekunde hazisimami, na mizunguko ya dunia, jua, na mwezi huendelea kwa kasi zaidi. Katika hisia zao, watu wanaamini kwamba siku hiyo haiko mbali sana, kama kwamba siku yao ya mwisho ipo mbele ya macho yao. Watu hutayarisha kila kitu bila kukoma kwa ajili ya wakati wao wa kifo, ili kutimiza kusudi wakati wa kufa kwao; la sivyo, wangekuwa wameishi bure, na je, hilo sio la kujutia? Wakati Mungu anaangamiza ulimwengu, Anaanza na mabadiliko katika masuala ya ndani ya nchi, ambapo hutokea mapinduzi; hivyo, Mungu huhamasisha huduma ya watu kote kote ulimwenguni. Nchi ambamo joka kubwa jekundu hulala likiwa limejiviringisha ni eneo la maonyesho. Kwa sababu, ndani, imepasuka, mambo yake ya ndani yameingia katika machafuko, kila mtu anafanya kazi ya kujitetea, akijitayarisha kukimbilia mwezini—lakini ni jinsi gani wanaweza kuepuka utawala wa mkono wa Mungu? Kama Mungu alivyosema tu kwamba watu “watakuwa kutoka kwenye kikombe chao kichungu.” Wakati wa ugomvi wa ndani ndio hasa wakati Mungu anaondoka duniani; Mungu hataendelea kukaa katika nchi ya joka kubwa jekundu, na Atamaliza kazi Yake duniani mara moja. Inaweza kusemwa kuwa wakati hukimbia, na hakuna muda mwingi uliobaki. Kutokana na sauti ya maneno ya Mungu inaweza kuonekana

kwamba tayari Mungu amenena kuhusu hatima ya wote kote kote ulimwenguni, kwamba Hana lolote la kusema kwa wakati uliosalia. Hilo ndilo Mungu anamfichulia mwanadamu. Ni kwa sababu ya lengo la Mungu kumuumba mwanadamu ndio Anasema “Machoni Pangu, mwanadamu ndiye mtawala wa vitu vyote. Nimempa mamlaka si haba, Nikimwezesha kusimamia vitu vyote duniani—nyasi iliyo juu ya milima, wanyama katika misitu, na samaki majini.” Mungu alipomuumba mwanadamu, Aliamua mbeleni kuwa mwanadamu angekuwa bwana wa vitu vyote—lakini mwanadamu alipotoshwa na Shetani, na hivyo hawezi kuishi jinsi ambavyo angetenda. Hili limesababisha ulimwengu wa leo, ambamo watu hawatofautiani na wanyama, na milima imechanganyika na mito, na matokeo ni kwamba “Maisha yake yote ni yale ya maumivu makali, na kukimbia hapa na pale, na raha kuongezwa kwa utupu.” Kwa sababu hakuna maana kwa maisha ya mwanadamu, na kwa sababu hili halikuwa lengo la Mungu katika kumuumba mwanadamu, ulimwengu wote umevurugika. Wakati Mungu ataweka ulimwengu wote kwa utaratibu, watu wote wataanza rasmi kupitia maisha ya mwanadamu, na wakati huo tu ndipo maisha yao yataanza kuwa na maana. Watu wataanza kutumia mamlaka waliyopewa na Mungu, wataonekana rasmi mbele ya vitu vyote kama bwana wao, na watakubali uongozi wa Mungu duniani, na hawatamuasi Mungu tena bali watamtii Mungu. Watu wa leo, hata hivyo, wako mbali sana na hilo. Yote wafanyayo tu ni “kupata pesa kwa njia ya udanganyifu” kupitia kwa Mungu, na kwa hiyo Mungu anauliza msururu wa maswali kama vile “Je, kazi Ninayofanya kwa mwanadamu haina faida yoyote kwake?” Kama Mungu hakuuliza maswali haya, hakuna kile ambacho kingefanyika; lakini wakati Anauliza mambo kama hayo, watu wengine hawawezi kusimama imara, kwa sababu kuna kuwiwa katika dhamiri zao, na sio kwa ajili ya Mungu kabisa, bali kwao wenyewe. Mambo yote ni matupu: hivyo, watu hawa na “watu wa kila dini, nyanja ya jamii, taifa, na dhehebu wote wanajua utupu ulio duniani, na wote wananitafuta na kungoja kurejea Kwangu.” Watu wote wanatamani sana kurudi kwa Mungu ili Aweze kukomesha enzi ya kale ya utupu, lakini pia wanaogopa kuingia katika maafa. Ulimwengu mzima wa dini utabaki ukiwa mara moja, na kutotunzwa na wote; hawana ukweli, na watatambua kwamba imani yao kwa Mungu sio dhahiri nayo ni dhahania. Watu wa kila eneo la jamii pia watatawanyika, na kila taifa na dhehebu litaanza kuangukia msukosuko. Kwa kifupi, ukawaida wa mambo yote utatenganishwa, yote yatapoteza ukawaida wake, na kwa hiyo, pia, watu watafichua nyuso zao za kweli. Hivyo Mungu anasema, “Wakati mwingi sana Nimepaza sauti Nikimwita mwanadamu, lakini je, kuna yule ambaye amehisi huruma? Je, kuna yeyote ambaye amewahi kuishi katika ubinadamu? Mwanadamu anaweza kuishi katika mwili, lakini hana ubinadamu. Je, alizaliwa katika ufalme wa wanyama?” Mabadiliko pia yanatokea miongoni mwa wanadamu, na kwa sababu ya mabadiliko haya kila mmoja anaainishwa kulingana na aina. Hii ni kazi ya Mungu katika siku za mwisho, na athari ambayo inapaswa kutimizwa kwa kazi ya siku za mwisho. Mungu anavyozidi kuzungumzia waziwazi kiini cha mwanadamu, hivyo

inathibitishwa kuwa mwisho wa kazi Yake unakaribia, na zaidi ya hayo kuwa Mungu amejificha zaidi kutoka kwa watu, ambalo huwafanya wahisi kubabaika zaidi. Kadri watu wanavyozingatia mapenzi ya Mungu kwa kiasi kidogo, ndivyo wanavyozingatia kazi ya Mungu ya siku za mwisho kwa kiasi kidogo; hili huwazuia kutoingilia, na hivyo Mungu hufanya kazi ambayo Ananuia kuifanya wakati hakuna mtu anayezingatia. Hii ni kanuni moja ya kazi ya Mungu kotekote katika enzi. Kadri anavyozingatia udhaifu wa watu kwa kiasi kidogo, hivyo inaonyeshwa kuwa uungu wa Mungu ni wazi zaidi, na hivyo siku ya Mungu inakaribia.

Sura ya 26

Kutoka kwa maneno yote yaliyonenwa na Mungu, inaweza kuonekana kwamba siku ya Mungu inakaribia kila siku inapopita. Ni kama kwamba siku hii iko mbele ya macho ya watu, kama kwamba itafika kesho. Hivyo, baada ya kusoma maneno ya Mungu, watu wote wanajawa na hofu, na pia wana hisia kiasi fulani ya ukiwa wa dunia. Ni kama kwamba, jinsi majani yanavyoanguka na manyunu kushuka, watu wote wametoweka wasionekane tena, kama kwamba wote wametoweka kabisa. Kila mtu ana hisia ya kuogofya, na ingawa wote wanajitahidi sana, na wanataka kuridhisha malengo ya Mungu, wote wakitumia kila nguvu waliyo nayo kutimiza nia ya Mungu ili mapenzi ya Mungu yaweze kuendelea sawasawa, bila kizuizi, hisia kama hiyo kila mara huchanganyika na hisia ya kuogofya. Chukua matamko ya leo: Kama yangeenezwa kwa umma, yakatangazwa kwa ulimwengu wote, basi watu wote wangeinamishwa vichwa vyao na kulia, kwani katika maneno “Nitaiangalia dunia yote, na, Nikitokea Mashariki ya dunia na haki, adhama, ghadhabu, na kuadibu, Nitajionyesha kwa wanadamu wengi wa tabaka mbalimbali!” wote wanaoelewa mambo ya kiroho wanaona kwamba hakuna mtu anayeweza kuhepa kuadibu kwa Mungu, kwamba wote watafuata aina yao wenyewe baada ya kupitia mateso ya kuadibu. Kwa kweli, hii ni hatua ya kazi ya Mungu, na hakuna mtu anayeweza kuibadilisha. Wakati Mungu aliumba ulimwengu, Alipowaongoza wanadamu, Alionyesha hekima na ajabu Yake, na Anapoikomesha enzi hii tu ndio watu wanaona haki Yake ya kweli, uadhama, ghadhabu, na kuadibu. Zaidi ya hayo, ni kwa njia ya kuadibu tu ndio wanaweza kuona haki, uadhama, na ghadhabu Yake; hii ni njia ambayo inapaswa kufuatwa, kama vile, katika siku za mwisho, kupata mwili kwa Mungu ni muhimu, na ni ya lazima. Baada ya kutangaza mwisho wa wanadamu wote, Mungu anamwonyesha mwanadamu kazi Anayoifanya leo. Kwa mfano, Mungu anasema, “Israeli ya kitambo haiko tena, na Israeli ya leo imeamka, imara na kama mnara, katika dunia, imesimama katika mioyo ya binadamu wote. Israeli ya leo kwa hakika itapata chanzo cha kuwepo kupitia kwa watu Wangu!” “Aa, Misri yenye chuki! ... Mtakosaje kuwa katika kuadibu Kwangu?” Mungu kwa makusudi Anawaonyesha watu matunda yaliyopatikana na nchi mbili zilizo kinyume kutoka kwa mikono ya Mungu, kwa hali moja Akitaja Israeli, ambayo ni yakinifu, na kwa hali nyingine Akiashiria wateule wote wa Mungu—

ambalo ni kusema, jinsi wateule wa Mungu wanavyobadilika jinsi Israeli inavyobadilika. Wakati Israeli imerejelea kabisa umbo lake la asili, wateule wote watafanywa wakamilifu baadaye—ambalo ni kusema, Israeli ni ishara ya maana ya wale ambao Mungu anawapenda. Misri, wakati huo huo, ni kukutana kwa wawakilishi wa wale ambao Mungu anawachukia. Inavyozidi kuoza, ndivyo wale wanaochukiwa na Mungu wanavyozidi kuwa wapotovu—na baadaye Babeli inaanguka. Hii inafanya tofauti ya wazi. Kwa kutangaza miisho ya Israeli na Misri, Mungu anafichua hatima ya watu wote; hivyo, Anapotaja Israeli, Mungu pia Anazungumza kuhusu Misri. Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba siku ya uharibifu wa Misri ni tarehe ya maangamizo ya ulimwengu, tarehe ambayo Mungu anawaadibu watu wote. Hili litatokea hivi karibuni; liko karibu kufanikishwa na Mungu, na ni kitu ambacho hakionekani kabisa na jicho la mwanadamu, lakini pia ni cha lazima, na hakiwezi kubadilishwa na mtu yeyote. Mungu anasema, “wale wote wanaosimama dhidi Yangu wataadhibiwa na Mimi milele kwa hakika. Kwani Mimi ni Mungu mwenye wivu, Sitawasamehe wanadamu kwa urahisi kwa yote ambayo wametenda.” Kwa nini Mungu anazungumza kwa masharti haya kamili? Na kwa nini Yeye mwenyewe Amapata mwili katika taifa la joka kuu jekundu? Kutoka kwa maneno ya Mungu lengo Lake linaweza kuonekana: Hakuja kuwaokoa watu, au kuwaonyesha huruma, au kuwatunza, au kuwalinda—bali kuwaadibu wale wote wanaompinga Yeye. Kwa maana Mungu anasema, “Hakuna anayeweza kuhepa kuadibu Kwangu.” Mungu anaishi katika mwili, na, zaidi ya hayo, Yeye ni mtu wa kawaida—hata hivyo Hawasamehei watu kwa udhaifu wao kwa kutoweza kumjua Yeye kwa udhahania; badala yake, kwa sababu Yeye ni wa kawaida, Anawashutumu watu kwa dhambi zao zote, Anawafanya wale wote wanaouona mwili wake kuwa wale wanaoadibiwa, na hivyo wanakuwa sadaka kwa niaba ya wale wote ambao sio watu wa taifa la joka kuu jekundu. Lakini hii siyo mojawapo ya malengo ya msingi ya kupata mwili kwa Mungu. Mungu alipata mwili kimsingi ili Apigane vita, katika mwili, na joka kuu jekundu, na kuleta aibu kwalo kupitia vita. Kwa sababu nguvu kuu ya Mungu inadhihirishwa zaidi kwa kupambana na joka kuu jekundu katika mwili kuliko katika Roho, Mungu hupigana katika mwili ili kuonyesha matendo na kudura Yake. Kwa sababu ya kupata mwili kwa Mungu, watu wengi mno wameshutumiwa “bila hatia”, watu wengi mno wametupwa jehanamu, na kutupwa katika kuadibu, wakiteseka katika mwili. Hili ni dhihirisho la tabia ya haki ya Mungu, na bila kujali jinsi wale wanaompinga Mungu wanavyobadilika leo, tabia adilifu ya Mungu haitabadilika kamwe. Kwa kushutumiwa mara moja, watu wanashutumiwa milele, na wasiweze kamwe kuinuka tena. Tabia ya mwanadamu haiwezi kuwa kama ya Mungu. Kwa wale wanaompinga Mungu, watu huwa moto na baridi kwa zamu, wanayumbayumba kushoto na kulia, wanaenda juu na chini, hawawezi kubaki vilevile wakati wote, wakati mwingine wakichukiwa kabisa, wakati mwingine wakishikiliwa kwa karibu; hali za leo zimetokea kwa sababu watu hawajui kazi ya Mungu. Kwa nini Mungu anasema maneno kama vile, “Malaika ni, hata hivyo, malaika;

Mungu, hata hivyo, ni Mungu; pepo ni, hata hivyo, pepo; Wadhalimu bado ni wadhalimu; na watakatifu bado ni watakatifu”? Je, huwezi kulielewa? Je, yawezekana kwamba Mungu amekumbuka visivyo? Hivyo, Mungu anasema, “kila mtu anatengwa kulingana na aina yake, na kutafuta njia bila kujua wanajipata wakirejea katika ngome za familia zao.” Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba leo, tayari Mungu ameanisha vitu vyote katika familia zao, ili usiwe tena “ulimwengu usio na mwisho,” na watu wasile tena kutoka kwenye chungu kimoja kikubwa, bali watekeleze kazi zao wenyewe nyumbani kwao, wakitekeleza wajibu wao wenyewe. Huu ulikuwa mpango wa asili wa Mungu wakati wa uumbaji wa ulimwengu; baada ya kuainishwa kulingana na aina, watu “wangekula chakula chao wenyewe”—Mungu angeanza hukumu. Kutokana na hilo, maneno haya yalitoka kinywani mwa Mungu: “Nitarejesha hali ya awali ya uumbaji, Nitarejesha kila kitu kiwe katika hali ya awali, Nikibadilisha kila kitu kwa namna kubwa, ili kila kitu kirudi ndani ya mpango Wangu.” Hilo ndilo lengo halisi la kazi yote ya Mungu, na si vigumu kulielewa. Mungu atakamilisha kazi Yake—mtu angeweza kuizuia kazi Yake? Na Mungu angeweza kuchana agano lililowekwa kati Yake na mwanadamu? Ni nani anayeweza kubadilisha kile kinachofanyika na Roho wa Mungu? Angeweza kuwa mtu yeyote miongoni mwa wanadamu?

Zamani, watu walielewa kwamba kulikuwa na sheria kwa maneno ya Mungu: Mara tu Mungu aliponena, ukweli ulifanikishwa punde. Hakuna uongo katika hili. Kwa kuwa Mungu amesema Atawaadibu watu wote, na, zaidi ya hayo, kwa kuwa Ametoa amri za utawala, inaweza kuonekana kwamba kazi ya Mungu imetekelezwa kwa kiwango fulani. Katiba iliyotolewa kwa watu wote hapo zamani ililenga maisha yao na mtazamo wao kwa Mungu. Haikufikia asili; haikusema kwamba ilitegemea majaliwa ya Mungu, bali kwa tabia ya mwanadamu wakati huo. Amri za utawala za leo ni za pekee, zinazungumzia jinsi “Binadamu wote watafuata aina yao, na watapokea kuadibu kunakotofautiana kulingana na kile walichofanya.” Bila kusoma kwa makini, hakuna tatizo linaloweza kupatikana katika hili. Kwa sababu ni katika enzi ya mwisho tu ndio Mungu anafanya vitu vyote vifuata aina yao wenyewe, baada ya kusoma hili watu wengi hubaki wamekanganywa na kuchanganyikiwa, bado ni vuguvugu, hawaoni umuhimu wa nyakati, na hivyo hawachukulii hili kama onyo. Kwa nini, kwa wakati huu, amri za utawala wa Mungu—ambazo zinatangazwa kwa ulimwengu wote—zinaonyeshwa kwa mwanadamu? Je, hawa watu wanawakilisha wale wote walio kote kote ulimwenguni? Yawezekana kwamba, baadaye, zaidi, Mungu anaongeza huruma kwa watu hawa? Je, watu hawa wamekuwa na vichwa viwili? Wakati Mungu anawaadibu watu wa ulimwengu wote, wakati maafa ya kila aina yanapofika, kutokana na maafa haya, mabadiliko yatatokea kwenye jua na mwezi, na wakati misiba hii itakapomalizika, jua na mwezi vitakuwa vimebadilishwa—na huu unaitwa mpito. Inatosha kusema, maafa ya siku zijazo yatakuwa ya kusikitisha. Usiku unaweza kuchukua nafasi ya

mchana, jua linaweza kutoonekana kwa mwaka, kunaweza kuwa na miezi kadhaa ya joto la kuunguza, mwezi unaopotea unaweza kumkabili wanadamu daima, kunaweza kuonekana hali ya ajabu ya jua na mwezi kuchomoza pamoja, n.k. Kufuatia mabadiliko kadhaa ya mafuatano, hatimaye, baada ya kupita kwa muda, yatafanywa upya. Mungu huzingatia sana mipango ya wale ambao ni wa shetani. Hivyo, Anasema kwa makusudi, “Kati ya binadamu walio ulimwenguni, wale wote walio wa shetani wataangamizwa.” Wakati “watu” hawa bado hawajaonyesha tabia zao halisi, daima Mungu hutumia huduma zao; kutokana na hilo, Hazingatii matendo yao, Yeye hawapatii “thawabu” wanapofanya mema, wala Hapunguzi “mishahara” wanapofanya vibaya. Kwa hivyo, Yeye huwapuuza, Hawathamini. Habadiliki ghafla kwa sababu ya “wema” wao, kwani haijalishi wakati au mahali, asili ya mwanadamu haibadiliki, kama tu agano lililoanzishwa kati ya Mungu na mwanadamu, kama vile, mwanadamu asemavyo, “hakutakuwa na mabadiliko hata kama bahari zitakauka na miamba ivunjike.” Hivyo, Mungu huwaainisha tu watu hao na Hawasikilizi kwa urahisi. Kutoka wakati wa uumbaji hadi leo, shetani hajawahi kujistahi vizuri. Kila mara, yeye amepinga, amechafua, na kutokubali. Mungu anapotenda au kunena, daima yeye hujaribu kushiriki—lakini Mungu hamtambui. Kwa kumtaja shetani, ghadhabu ya Mungu inabubujika, bila kuzuilika; kwa sababu yeye si kitu kimoja na Roho, hakuna uhusiano, bali umbali na utengano tu. Kufuatia ufichuzi wa mihuri saba, hali ya dunia inazidi kuwa matatani, vitu vyote “vinaendelea bega kwa bega na mihuri saba,” bila kubaki nyuma hata kidogo. Kote kote katika maneno ya Mungu, Mungu anawatazama watu kama walioduwazwa, lakini hawajaamka kamwe. Ili kufikia kiwango cha juu, ili kuonyesha nguvu za watu wote, na zaidi ya hayo, ili kuihitimisha kazi ya Mungu katika kilele chake, Mungu anawauliza watu msururu wa maswali, kama kwamba Anapanua matumbo yao, na hivyo Anawajaza tena watu wote. Kwa sababu watu hawa hawana kimo halisi, kulingana na mazingira halisi, wale ambao wanajazwa ni bidhaa ambazo zinazofikia kiwango, na wale ambao hawajajazwa ni takataka isiyofaa. Haya ni matakwa ya Mungu kwa mwanadamu, na lengo la njia ambayo kwayo Anaizungumzia. Hasa, wakati Mungu anasema “Je, yawezekana kwamba Mimi, Nikiwa duniani, Siko sawa na Mimi niliye mbinguni? Je, yawezekana kwamba Mimi, Ninapokuwa mbinguni, Siwezi kushuka chini duniani? Je, yawezekana kwamba Mimi, Nikiwa duniani, Sistahili kustahimili hadi mbinguni?” maswali haya huendelea kuwafanya watu wamjue Mungu hata zaidi. Kutoka kwa maneno ya Mungu, makusudi ya dharura ya Mungu inaonekana; watu hawawezi kuyafikia, na Mungu Anaongeza masharti tena na tena, hivyo Akiwakumbusha watu wote wamjue Mungu wa mbinguni Aliye duniani, na kumjua Mungu aliye mbinguni lakini Anaishi duniani.

Kutokana na maneno ya Mungu hali za mwanadamu zinaweza kuonekana: “Wanadamu wote wanaweka bidii kwa maneno Yangu, wakifanya uchunguzi wao wenyewe kuhusu sura

Yangu ya nje, lakini wote wanashindwa, bila matokeo yoyote ya kuonyesha, badala yake, wanaangushwa na maneno Yangu na hawawezi kuthubutu kusimama tena.” Nani anaweza kuelewa huzuni ya Mungu? Nani anaweza kuufaraji moyo wa Mungu? Ni nani anayeupendeza moyo wa Mungu katika kile ambacho Mungu anataka? Wakati watu hawatoi matokeo, wanajikana na kwa kweli wako chini ya mipango ya Mungu. Hatua kwa hatua, wanapoionyesha mioyo yao ya kweli, kila mmoja hufuata aina yake mwenyewe, na hivyo inaonekana kwamba asili ya malaika ni utii mtakatifu kwa Mungu. Na kwa hiyo, Mungu anasema, “Binadamu wanafunuliwa katika hali yao halisi.” Kazi ya Mungu inapofikia hatua hii, kazi yote ya Mungu itakuwa imekamili. Mungu anaonekana kutoesema chochote kuhusu Yeye kuwa mfano wa wanawe na watu wake, badala yake Akilenga kuwafanya watu wote kuonyesha umbo lao la asili. Je, unaelewa maana halisi ya maneno haya?

Sura ya 27

Leo, maneno ya Mungu yamefikia kilele chake, ambako ni kusema, sehemu ya pili ya enzi ya hukumu imefikia kilele chake. Lakini sio kilele cha juu kabisa. Wakati huu, sauti ya Mungu imebadilika, si ya kudhihaki wala ya ucheshi, na haigongi au kulaani; Mungu ametuliza sauti ya maneno Yake. Sasa, Mungu anaanza “kubadilishana maoni” na mwanadamu. Mungu anaendelea kazi ya enzi ya hukumu na pia kufungua njia ya sehemu inayofuata ya kazi, ili sehemu zote za kazi Yake zipatane. Kwa upande mmoja, Anasema kuhusu “ukaidi na uhalifu sugu wa mwanadamu,” na kwa upande mwingine, Anasema “katika furaha na huzuni ya kutengana na kuunganika Kwangu na mwanadamu”—vyote viwili vinachochea mjibizo katika mioyo ya watu, vikiigusa hata mioyo iliyo baridi kabisa ya binadamu. Lengo la Mungu katika kusema maneno haya hasa ni kuwafanya watu wote waanguke chini mbele za Mungu, bila mnong’ono, mwisho kabisa, na baadaye tu “ndipo matendo Yangu hudhihirika, na kumfanya kila mmoja, katika upotovu wake, kunitambua Mimi.” Ufahamu kuhusu Mungu wa watu wa kipindi hiki unasalia wa juujuu kabisa, sio ufahamu wa kweli. Ingawa wanajikakamua kadri wawezavyo, hawawezi kufikia mapenzi ya Mungu; leo, maneno ya Mungu yamefikia upeo wake, lakini watu wanabakia katika hatua za mwanzo, na hivyo hawawezi kuingia katika matamko ya sasa hivi—ambalo linaonyesha kuwa Mungu na mtu ni tofauti kabisa. Kulingana na hili, wakati maneno ya Mungu yatatamalizika watu wataweza tu kufikia viwango vya chini zaidi vya Mungu. Hii ndio njia ambayo Mungu hufanya kazi ndani ya watu hawa ambao wamepotoshwa kabisa na joka kubwa jekundu, na Mungu lazima afanye hivyo ili Atimize matokeo bora kabisa. Watu wa makanisa huzingatia maneno ya Mungu kiasi kidogo zaidi, lakini nia ya Mungu ni kwamba waweze kumjua Mungu katika maneno Yake—je, tofauti haipo? Hata hivyo, jinsi mambo yalivyo, Mungu hajali tena kuhusu udhaifu wa mwanadamu, na Anaendelea kusema bila kujali kama watu wanaweza kukubali maneno Yake au la. Kulingana na nia Yake, wakati maneno Yake

yatamalizika utakuwa wakati ambapo kazi Yake duniani itakamilika. Lakini kazi hii ni tofauti na ya zamani. Wakati matamko ya Mungu yatamalizika, hakuna mtu atakayejua; wakati kazi ya Mungu itafika mwisho, hakuna mtu atakayejua; na wakati umbo la Mungu litabadilika, hakuna mtu atakayejua. Hivyo ndivyo hekima ya Mungu ilivyo. Ili kuepuka mashtaka yoyote kutoka kwa Shetani na kuingiliwa kokote na nguvu za uhasama, Mungu hufanya kazi bila mtu yeyote kujua, na wakati huu hakuna mjibizo miongoni mwa watu wa dunia. Ijapokuwa ishara za kugeuka sura kwa Mungu zilizungumziwa wakati mmoja, hakuna mtu anayeweza kulitambua hili, kwa kuwa mwanadamu amesahau jambo hili, naye halizingatii. Na kwa sababu ya mashambulizi kutoka ndani na nje—maafa ya ulimwengu wa nje na kuchomwa na kutakaswa na maneno ya Mungu—watu hawako radhi tena kumfanyia Mungu kazi, kwa sababu wanashughulika sana na shughuli zao wenyewe. Wakati watu wote wanakana ufahamu na ufukuziaji wa zamani, wakati watu wote wamejiona kwa dhahiri, watashindwa na nafsi zao wenyewe hazitakuwa na nafasi tena mioyoni mwao. Wakati huo tu ndio watu watatamani maneno ya Mungu kwa kweli, wakati huo tu ndio maneno ya Mungu yatakuwa na nafasi kweli katika mioyo yao, na wakati huo tu ndio maneno haya yatakuwa yamekuwa chanzo cha kuwepo kwao—na wakati huu, mapenzi ya Mungu yatakuwa yametimizwa. Lakini watu wa leo wako mbali sana na hilo. Baadhi yao wameweza kusonga kwa shida, na hivyo Mungu anasema huu ni “ukaidi sugu.”

Maneno yote ya Mungu yana maswali mengi. Kwa nini Mungu anaendelea kuuliza maswali kama hayo? “Mbona wasitubu dhambi zao na kuzaliwa mara ya pili? Mbona binadamu hupenda kuishi kwenye chemichemi badala ya kuishi mahali pasipo na matope? ...” Zamani, Mungu alifanya kazi kwa njia ya kuelezea mambo moja kwa moja au kuwa wazi moja kwa moja. Lakini baada ya watu kupitia maumivu mengi, hivyo Mungu hakuzungumza moja kwa moja. Kwa upande mmoja, watu wanaona kasoro zao wenyewe katika maswali haya, na kwa upande mwingine, wanafahamu njia ya kufanya mazoezi. Kwa sababu watu wote hupenda kula kile kinachopatikana kwa urahisi, Mungu ananena kama yanavyostahili mahitaji yao, Akiwapa mada za kutafakari, ili waweze kuzitafakari. Hii ni hali moja ya umuhimu wa maswali ya Mungu. Kwa kawaida, huu sio umuhimu wa baadhi ya maswali Yake, kwa mfano: “Inawezekana kuwa Mimi Nimewadhulumu? Inawezekana kuwa Mimi Nimewapotosha? Inawezekana kuwa Mimi nimewaelekeza kuzimu?” Maswali kama haya huonyesha dhana zilizo katika vina vya mioyo ya watu. Ingawa midomo yao haisemi, kuna shaka ndani ya mioyo ya wengi wao, na wanaamini kwamba maneno ya Mungu yanawafafanua kama wasiokuwa na faida. Kwa kawaida, watu kama hao hawajijui, lakini hatimaye, watakubali kushindwa na maneno ya Mungu—hili haliepukiki. Kufuatia maswali haya, Mungu anasema pia “Nakusudia kusambaratisha mataifa yote yatawanyike, sembuse familia ya mwanadamu.” Watu wanapolikubali jina la Mungu, hivyo

mataifa yote yatatetemeka, watu watabadili mawazo yao polepole, na katika familia mahusiano kati ya baba na mwana, mama na binti au mume na mke yatakoma kuwapo. Zaidi ya hayo, mahusiano kati ya watu katika familia yatakuwa ya kufarakana zaidi; watajiunga na familia kubwa, na ukawaida wa maisha ya takriban familia zote utatenganishwa. Na kwa sababu ya hili, dhana ya familia katika mioyo ya watu itazidi kuwa ya wasiwasi.

Kwa nini, katika maneno ya Mungu ya leo, mengi sana yametolewa kwa “kubadilishana hisia za moyoni” na watu? Kwa kawaida, hili pia ni kwa ajili ya kutimiza matokeo fulani, ambayo kutoka kwayo inaweza kuonekana kwamba moyo wa Mungu umejaa wasiwasi. Mungu anasema, “Nionapo huzuni, nani anaweza kunifariji kwa moyo wake?” Mungu anasema maneno haya kwa sababu moyo Wake umelemewa na huzuni. Kwa sababu watu hawawezi kuyajali kabisa mapenzi ya Mungu, na daima huwa ni wapotovu, na hawawezi kujizuia—wanafanya wapendavyo; kwa sababu wao ni duni sana, na daima wao hujisamehe, na hawajali kuhusu mapenzi ya Mungu. Lakini kwa sababu watu wamepotoshwa na Shetani hadi leo, na hawawezi kujikomboa, Mungu anasema: “Wanawezaje kuepuka kutoka kwa midomo ya mbwa mwitu mlafi? Wanawezaje kujiokoa kutokana na tishio na majaribu yake?” Watu wanaishi katika mwili—katika kinywa cha mbwa mwitu mlafi. Kwa sababu ya hili, na kwa sababu watu hawajijui na daima wao hujiendeka na kujiingiza katika uzinzi, Mungu hana budi kuhisi wasiwasi. Kadiri Mungu anavyowakumbusha watu hivyo, ndivyo wanavyohisi bora zaidi mioyoni mwao, na ndivyo wanavyokuwa radhi zaidi kushirikiana na Mungu. Wakati huo tu ndipo mwanadamu na Mungu watapatana, bila utengano wowote au umbali kati yao. Leo, wanadamu wote wanasubiri ujio wa siku ya Mungu, na kwa hiyo wanadamu hawajawahi kusonga mbele. Lakini Mungu anasema: “Wakati ambapo Jua la haki litaonekana, Mashariki itaangazwa, kisha litaangaza ulimwenguni kote, likimfikia kila mtu.” Kwa maneno mengine, wakati Mungu atabadili umbo Lake, Mashariki itaangazwa kwanza na nchi ya Mashariki itakuwa ya kwanza kuchukua nafasi yake, baada ya hapo nchi zilizobaki zitafanywa upya kutoka kusini hadi kaskazini. Huu ndio utaratibu, na yote yatakuwa kwa mujibu wa maneno ya Mungu, na mara tu awamu hii itakapokuwa imekamilishwa watu wote wataona. Mungu hufanya kazi kulingana na utaratibu huu. Watakapoiona siku hii, watu watafurahi sana. Inaweza kuonekana kutoka kwa nia muhimu ya Mungu kwamba siku hii haiko mbali sana.

Katika maneno ya leo, sehemu ya pili na ya tatu zinachochea machozi ya uchungu kwa wote wanaompenda Mungu. Mioyo yao imegubikwa kivulini mara moja, na tangu wakati huu na kuendelea watu wote wamejaa huzuni kubwa mno kwa sababu ya moyo wa Mungu—baada tu ya Mungu kumaliza kazi Yake duniani, watahisi utulivu. Huu ni mwenendo wa kawaida. “Hasira inainuka ndani ya moyo Wangu, ikiandamana na hisia ya huzuni inayotapakaa. Wakati macho Yangu yanaangalia matendo ya watu na kila neno lao na kitendo kuwa vichafu, ghadhabu Yangu

huzidi, na moyoni Mwangu kuna hali kubwa zaidi ya udhalimu wa ulimwengu wa mwanadamu, ambalo linanifanya kuwa na huzuni zaidi; Natamani kuumaliza mwili wa mwanadamu mara moja. Sijui kwa nini mwanadamu hawezi kujitakasa katika mwili, kwa nini mwanadamu hawezi kujipenda katika mwili. Yawezekana kwamba ‘kazi’ ya mwili ni kubwa sana?” Katika maneno ya Mungu leo, Mungu amemfichulia mwanadamu hadharani wasiwasi wote ulio ndani ya moyo Wake, bila kuficha chochote. Wakati malaika wa mbingu ya tatu wanamchezea muziki na kumpigia vibati, Mungu bado anawatamani sana watu walio duniani, na ni kwa ajili ya hili ndipo Anasema “Malaika wanapocheza muziki wakinisifu, hii inasisimua huruma kwa ajili ya binadamu. Moyo wangu unajawa na huzuni ghafla, na inakuwa vigumu kujiondoa katika hisia hii ya kuhuzunisha.” Ni kwa sababu hii ndio Mungu anasema maneno haya: “Nitarekebisha udhalimu katika dunia ya mwanadamu. Nitafanya kazi Yangu kwa mikono Yangu mwenyewe ulimwenguni kote, Nikimkomesha Shetani asiwadharu watu Wangu tena, Nikiwakomesha maadui wasifanye kile wapendacho tena. Nitakuwa Mfalme duniani na kukipeleka kiti Changu cha enzi huko, na kuwafanya maadui waanguke chini na kukiri makosa yao mbele Yangu.” Huzuni ya Mungu inaongeza chuki Yake kwa pepo, na hivyo Anafichua mwisho wao kwa umati mapema. Hii ni kazi ya Mungu. Daima Mungu ametaka kuunganishwa tena na watu wote na kuimaliza enzi ya kale. Watu wote kote duniani wanaanza kusonga—ambalo ni kusema, watu wote chini ya dunia wanaingia katika uongozi wa Mungu. Kwa hiyo, mawazo yao yanageuka na kuwachukia wafalme wao. Punde si punde, watu wa dunia wataingia katika machafuko na wakuu wa nchi zote watakimbia kwenda kila upande, hatimaye watu wao watawaingiza kwenye bamba la kukata kichwa. Huu ndio mwisho kabisa wa wafalme wa pepo; hatimaye, hakuna mtu atakayeweza kutoroka, wote lazima waupitie. Leo, wale ambao ni “wajanja” wameanza kujiuzulu. Wanapona kwamba mambo hayaonekani kuwa mazuri, wanatumia fursa hii kusalimu amri na kutoroka shida ya msiba. Lakini Nasema wazi, kazi ambayo Mungu anafanya katika siku za mwisho ni hasa kumwadibu mwanadamu, kwa hiyo watu hawa wangewezaje kutoroka? Leo ni hatua ya kwanza. Siku moja, wote kote ulimwenguni wataingia katika ghasia ya vita, watu wa dunia hawatakuwa na viongozi tena, ulimwengu wote utakuwa kama rundo la mchanga uliochimbuliwa, usioongozwa na mtu yeyote, na watu watayajali tu maisha yao wenyewe, bila kumjali mtu mwingine yeyote, kwani kila kitu kinadhibitiwa na mkono wa Mungu—ndiyo maana Mungu anasema, “binadamu wote wanayagawanya mataifa mengine kulingana na mapenzi Yangu.” “Tarumbeta za malaika” ambazo Mungu anazungumzia sasa ni ishara, zinamwonya mwanadamu, na wakati tarumbeta zitalia mara nyingine, siku ya mwisho ya dunia itakuwa imefika. Wakati huo, kuadibu kote kwa Mungu kutaifika duniani kwa ukamilifu wake; hii itakuwa hukumu katili, na kuanza rasmi kwa nyakati za kuadibu. Miongoni mwa Waisraeli, mara nyingi kutakuwa na sauti ya Mungu ili kuwaongoza kupitia mazingira tofauti, na pia malaika wataonekana kwao. Waisraeli

watakamilishwa katika miezi michache tu, kwa sababu hawatastahili kupitia hatua ya kuondoa sumu ya joka kubwa jekundu, itakuwa rahisi kwao kuingia kwenye njia sahihi chini ya aina mbalimbali ya uongozi. Kutokana na maendeleo yaliyo Israeli inaweza kuonekana hali ya ulimwengu wote, na hii inaonyesha jinsi hatua za kazi ya Mungu zilivyo za haraka. “Wakati umewadia! Nitaianza kazi Yangu, Nitatawala miongoni mwa wanadamu!” Zamani, Mungu alitawala tu mbinguni. Leo, Anatawala duniani; Mungu amechukua mamlaka Yake yote, na hivyo inatabiriwa kuwa wanadamu wote hawatakuwa tena na maisha ya kawaida ya binadamu, kwa kuwa Mungu atapanga upya mbingu na dunia, na hakuna mtu anaruhusiwa kuingilia. Hivyo, mara nyingi Mungu humkumbusha mwanadamu kuwa “wakati umewadia.” Wakati Waisraeli wamekwisharudi katika nchi yao—siku ambayo nchi ya Israeli itakuwa imepatwa tena—kazi kubwa ya Mungu itakuwa imekamiliwa. Bila mtu yeyote kutambua, watu duniani kote wataasi, na nchi kote kote ulimwenguni zitaanguka kama nyota zilizo mbinguni; kufumba na kufumbua, zitakuwa magofu. Na baada ya kuwashughulikia, Mungu atajenga ufalme unaopendwa naye.

Sura ya 28

Hali ya watu ni kwamba kadri wanavyoelewa maneno ya Mungu kwa kiasi kidogo, ndivyo wanavyoshuku zaidi njia ya sasa ya Mungu ya kufanya kazi. Lakini hii haina athari kwa kazi ya Mungu; maneno Yake yanapofikia kiwango fulani, kwa kawaida mioyo ya watu itabadilika. Katika maisha yao, kila mtu huyakazia macho maneno ya Mungu, na pia wao huanza kutamani sana maneno Yake—na kwa sababu ya mfichuo wa Mungu wa siku zote, wanaanza kujidharau. Hata hivyo Mungu pia ametamka aina nyingi za maneno yafuatayo: “Wakati ameelewa maneno Yangu yote kwa undani, kimo cha mwanadamu kiko sawa na matakwa Yangu, na maombi yake yanazaa matunda, na sio bure au batili; Ninabariki maombi ya mwanadamu yaliyo ya kweli, na sio kujifanya.” Kwa kweli, watu hawawezi kuelewa kabisa maneno ya Mungu, wanaweza tu kuelewa juujuu. Mungu hutumia tu maneno haya kuwapa lengo la kufuatilia, ili kuwafanya wahisi kwamba Mungu hafanyi mambo kwa mzaha, lakini Yuko makini kuhusu kazi Yake, na ni wakati huo tu ndipo watakuwa na imani ya kufuatilia. Na kwa sababu watu wote huomba tu kwa ajili yao wenyewe, sio kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, lakini Mungu haghairi, maneno Yake daima yameelekezwa kwa asili ya mwanadamu. Ingawa watu wengi leo wanaomba, si waaminifu—ni kisingizio tu. Hali ya watu wote ni kwamba wao “wanauchukulia mdomo Wangu kama utoaji wa mambo mema ya namna maalum. Watu wote wanatamani kupata kitu kutoka kwenye kinywa Changu. Kama ni siri za taifa, au siri za mbinguni, au mienendo ya ulimwengu wa kiroho, au hatima ya mwanadamu.” Kwa sababu ya udadisi wao, watu wote wako tayari kutafuta vitu hivi, na hawataki kupata kitu chochote cha ruzuku ya maisha kutoka kwa maneno ya Mungu. Hivyo Mungu anasema, “Vitu vingi vinakosekana ndani ya mwanadamu: Hahitaji tu ‘nyongeza ya lishe’ bali ‘usaidizi wa kimawazo’ na ‘usambazaji wa lishe ya kiroho.’” Ni dhana

zilizo ndani ya watu ndizo zimesababisha uhasi wa leo, na ni kwa sababu macho yao ya kimwili ni “kikabaili” sana ndio maana hakuna nguvu kwa kile wanachosema na kufanya, na wao ni wazembe na wapurukushani katika mambo yote. Je, hizi si hali za watu? Je, watu hawapaswi kuharakisha na kurekebisha hili, badala ya kuendelea jinsi walivyo? Kuzijua siku za baadaye kuna faida gani kwa mwanadamu? Kwa nini watu huwa na athari baada ya kusoma baadhi ya maneno ya Mungu, lakini maneno Yake yaliyosalia hayana athari? Wakati Mungu anaposema, kwa mfano, “Ninatoa uponyaji kwa ugonjwa wa mwanadamu ili matokeo bora yatimizwe, ili watu wote wawe na afya nzuri, na ili, kupitia uponyaji Wangu warejeele hali ya kawaida,” inakuaje kwamba maneno haya hayana athari kwa watu? Je, kila kitu kinachofanywa na Mungu si kile kinachopaswa kutimizwa na mwanadamu? Mungu ana kazi ya kufanya—kwa nini watu hawana njia ya kutembea? Katika hili, je, hawamwachi Mungu? Kuna kazi nyingi kweli ambayo watu wanapaswa kufanya—kwa mfano, ni kiasi gani wanachojua kuhusu “joka kubwa jekundu” katika maneno “Je, mnalichukia kwa kweli lile joka kuu jekundu?” Maneno ya Mungu ya “Mbona Nimewauliza mara nyingi?” yanaonyesha kwamba bado watu hawajui asili ya joka kubwa jekundu, kwamba bado hawawezi kuingia ndani zaidi. Je, hii sio kazi ileile ambayo mtu anapaswa kufanya? Inawezaje kusemwa kwamba mwanadamu hana kazi? Ingekuwa hivyo, umuhimu wa Mungu kupata mwili ungekuwa upi? Je, Mungu anakuwa mzembe na mpurukushani kwa ajili ya kufanya mambo kwa namna isiyo ya dhati? Joka kubwa jekundu linaweza kushindwa kwa njia hii?

Mungu anasema, “Tayari Nimeanza, na Nitaanza hatua ya kwanza ya kazi Yangu ya kuadibu katika makazi ya joka kuu jekundu.” Maneno haya yanaelezwa kwa kazi iliyo katika uungu; watu wa leo tayari wameingia katika kuadibu mapema, na hivyo Mungu anasema hii ni hatua ya kwanza ya kazi Yake. Yeye hawafanyi watu wavumilie kuadibu kwa maafa, bali kule kwa maneno. Kwa sababu, wakati sauti ya maneno ya Mungu inabadilika, watu huwa wasiojua kabisa, baada ya hilo wote huingia katika kuadibu. Na mara wakishapitia kuadibu, ni kama tu anavyosema Mungu^[a] “Hivyo basi, mtatenda wajibu wenu kirasmi, na mtanisifu kirasmi kotekote katika nchi, milele na milele!” Hizi ni hatua katika kazi ya Mungu—hizi ni mpango Wake. Zaidi ya hayo, watu hawa wa Mungu wataona wenyewe mbinu ambazo kwazo joka kubwa jekundu linaadibiwa, hivyo msiba unaanza rasmi nje yake, katika ulimwengu unaowazingira. Hii ni mojawapo ya njia ambazo kwazo Mungu huwaokoa watu. Kwa ndani wanaadibiwa, na nje msiba unashuka kwa kishindo—huku ni kusema, maneno ya Mungu yanatimizwa. Kwa hivyo, watu wangependelea kupitia kuadibu badala ya msiba, na ni kwa sababu ya jambo hili ndio wanabaki. Kwa upande mmoja, hiki ni kiwango ambacho kazi ya Mungu imefikia; kwa upande mwingine, ni ili watu wote waweze kufahamu tabia ya Mungu. Hivyo Mungu anasema, “Wakati watu Wangu wananifurahia ni wakati joka kuu jekundu linaadibiwa. Kuwafanya watu wa joka kubwa

jekundu kusimama na kuliiasi joka ndiyo nia Yangu, na ndiyo njia ambayo Ninawakamilisha watu Wangu, na ni nafasi nzuri ya watu Wangu wote kukua maishani.” Ni kwa nini Mungu ananena maneno haya lakini hayawavutii watu?

Nchi ziko katika machafuko makubwa, kwa sababu fimbo ya Mungu imeanza kutimiza wajibu wake duniani. Kazi ya Mungu inaweza kuonekana katika hali ya dunia. Mungu anaposema “maji yatanguruma, milima itaanguka, mito mikuu itatawanyika,” hii ni kazi ya kwanza ya fimbo duniani, na matokeo yake ni kwamba “Nyumba zote duniani zitasambaratishwa, na mataifa yote duniani yatagawanywa; siku za marudiano kati ya mke na mume zitapita, mama na mwanawe hawatakutana tena, hakutakuwa tena na kuja pamoja kwa baba na bintiye. Nitayaharibu yote yaliyokuwa duniani.” Hiyo ndiyo itakuwa hali ya jumla ya familia duniani. Kwa kawaida, haingeweza kuwa hasa hali ya wote, lakini ni hali ya wengi wao. Kwa upande mwingine, inahusu hali ambazo watu wa mkondo huu wamepitia katika siku za baadaye. Inatabiri kwamba, mara wakishapitia kuadibu kwa maneno na wasioamini wamepatwa na msiba, hakutakuwa tena na mahusiano ya familia miongoni mwa watu duniani; wote watakuwa watu wa Sinim, na wote watakuwa waaminifu katika ufalme wa Mungu. Hivyo, siku za marudiano kati ya mke na mume zitapita, mama na mwanawe hawatakutana tena, hakutakuwa tena na kuja pamoja kwa baba na bintiye. Na kwa hiyo, familia za watu duniani zitatenganishwa, zitapasuliwa vipande vipande, na hii itakuwa kazi ya mwisho ambayo Mungu anafanya katika mwanadamu. Na kwa sababu Mungu ataeneza kazi hii kote kote ulimwenguni, Anachukua fursa ya kuwafafanulia watu neno “hisia,” hivyo Akiwawezesha kuona kwamba mapenzi ya Mungu ni kuzitenganisha familia zote za watu, na kuonyesha kwamba Mungu hutumia kuadibu ili kutatua migogoro yote ya familia miongoni mwa wanadamu. La sivyo, hapangekuwa na njia ya kuimaliza sehemu ya mwisho ya kazi ya Mungu duniani. Sehemu ya mwisho ya maneno ya Mungu huonyesha udhaifu mkubwa kabisa wa wanadamu—wote huishi katika hisia—na hivyo Mungu haepuki hata mmoja wao, na Hufunua siri zilizofichwa mioyoni mwa wanadamu wote. Kwa nini ni vigumu sana kwa watu kujitenga na hisia? Je, ni muhimu zaidi kuliko viwango vya dhamiri? Je, dhamiri inaweza kufanikisha mapenzi ya Mungu? Je, hisia inaweza kuwasaidia watu kupitia shida? Machoni pa Mungu, hisia ni adui Yake—hili halijanenwa wazi katika maneno ya Mungu?

Tanbihi:

a. Maandishi ya asili hayana maneno “ni kama tu anavyosema Mungu.”

Sura ya 29

Kati ya kazi inayofanywa na watu, baadhi yake hutekelezwa kwa maagizo ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu, lakini kwa sehemu yake Mungu hatoi maagizo ya wazi, ikionyesha

vya kutosha kwamba kile kinachofanywa na Mungu, leo, bado hakijafichuliwa kabisa—ambalo ni kusema, mengi bado yamefichwa na bado hayajajulikana na watu. Lakini mambo mengine yanahitaji kujulikana na watu, na kuna mwingine yanayohitaji kuwaacha watu wakiwa wamekanganywa na kuchanganyikiwa; hiki ndicho kinachohitajika na kazi ya Mungu. Kwa mfano, ujio wa Mungu kutoka mbinguni miongoni mwa mwanadamu: jinsi Alivyofika, Alifika kwa sekunde ipi, au kama mbingu na dunia na vitu vyote vilibadilika au la—mambo haya yanahitaji watu kuchanganyikiwa. Hili pia linategemea hali halisi, kwani mwili wa binadamu wenyewe hauwezi kuingia moja kwa moja katika ulimwengu wa kiroho. Hivyo, hata kama Mungu anasema wazi jinsi Alivyokuja duniani kutoka mbinguni, au wakati Anasema, “Siku hiyo ambayo vitu vyote vilifufuliwa, Nilikuja miongoni mwa wanadamu, na Nimeshinda naye kwa siku zilizokuwa za ajabu usiku na mchana,” maneno hayo ni kama mtu akilizungumzia shina la mti—hakuna athari hata kidogo, kwa sababu watu hawazijui hatua za kazi ya Mungu. Hata wakati wanapofahamu kweli, wanaamini kwamba Mungu alipaa kutoka mbinguni hadi duniani kama kichimbakazi na akazaliwa tena miongoni mwa wanadamu. Hili ndilo linalofikiwa na mawazo ya mwanadamu. Ni kwa sababu kiini cha mwanadamu ni kwamba hawezi kuelewa dutu ya Mungu, na hawezi kuelewa ukweli wa ulimwengu wa kiroho. Kwa asili yao pekee, watu hawangeweza kutenda kama mfano kwa wengine, kwa sababu watu wako sawa kwa asili, na si tofauti. Kwa hivyo, kuwataka watu waweze kuwa mfano wa wengine kufuata au kutumika kama mfano kinakuwa kitu kisicho na ukweli wa aina yoyote, inakuwa mvuke unaoinuka kutoka kwa maji. Ilhali Mungu anaposema, “anapata ujuzi fulani kuhusu kile Nilicho nacho na Nilicho,” maneno haya yanahutubiwa tu kwa dhihirisho la kazi ambayo Mungu anafanya katika mwili; kwa maneno mengine, yanaelekezwa kwa uso halisi wa Mungu—uungu, ambao hasa unahusu tabia Yake takatifu. Hiyo ni kusema, watu wanaulizwa kuelewa mambo kama vile kwa nini Mungu anafanya kazi kwa njia hii, ni mambo gani yanayohitajika kufanikishwa kwa maneno ya Mungu, kile ambacho Mungu anataka kutimiza duniani, kile Anachopenda kupata miongoni mwa wanadamu, mbinu ambazo kwazo Mungu hunena, na mtazamo wa Mungu kwa mwanadamu ni upi. Inaweza kusemwa kwamba hakuna kitu kinachostahili kujivunia katika mwanadamu, yaani, hakuna chochote ndani yake ambacho kinaweza kuonyesha mfano wa wengine kufuata.

Ni hasa kwa sababu ya ukawaida wa Mungu katika mwili, kwa sababu ya utofauti wa Mungu aliye mbinguni na Mungu aliye katika mwili, Asiyeonekana kuzaliwa na Mungu aliye mbinguni, ndio Mungu anasema, “Nimepita kati ya wanadamu kwa miaka mingi, lakini hajawahi kufahamu hili, na hajawahi kunijua.” Mungu anasema pia, “Wakati nyayo Zangu zitaunyaga ulimwengu mzima na hadi miisho ya dunia, mwanadamu ataanza kutafakari juu yake mwenyewe, na watu wote watakuja Kwangu na kusujudu mbele Zangu na kuniabudu. Hii

itakuwa siku ya utukufu Wangu, siku ya kurudi Kwangu, na pia siku ya kuondoka Kwangu.” Hii tu ndiyo siku ambayo uso halisi wa Mungu unaonyeshwa kwa mwanadamu. Hata hivyo Mungu hacheleweshi kazi Yake kama matokeo, na Yeye hufanya tu kazi ambayo inapaswa kufanyika. Wakati Anapohukumu, Anahukumu kulingana na mtazamo wa watu kwa Mungu aliye katika mwili. Hii ni mojawapo ya milolongo muhimu ya matamko ya Mungu wakati wa kipindi hiki. Kwa mfano, Mungu anasema, “Nimeanza kirasmi, katika ulimwengu wote, ukamilishaji wa mpango Wangu wa usimamizi. Kuanzia sasa na kuendelea, wowote ambao si waangalifu wanastahili kutumbukizwa katikati ya kuadibu kusiko na huruma wakati wowote.” Haya ni maudhui ya mpango wa Mungu, na sio yasiyo ya kawaida wala ya ajabu, lakini yote ni hatua ya kazi. Watu na wana wa Mungu walio ng’ambo, wakati huo huo, wanahukumikiwa na Mungu kulingana na yote wanayoyafanya katika makanisa, na hivyo Mungu asema, “Ninapofanya kazi, malaika wote wanaanzisha vita vya maamuzi na Mimi na kuamua kutimiza matakwa Yangu katika hatua ya mwisho, ili watu walio duniani wajitoe Kwangu kama malaika, na wasiwe na haja ya kunipinga Mimi, na wasifanye chochote ambacho kinaniasi. Hii ndio elimumwendo ya kazi Yangu kotekote katika ulimwengu.” Hii ni tofauti katika kazi ambayo Mungu hutekeleza kotekote duniani; Yeye hutumia hatua tofauti kulingana na wale wanaoelekezewa. Leo, watu wote wa makanisa wana mioyo yenye shauku, na wameanza kula na kunywa maneno ya Mungu—ambalo linatosha kuonyesha kwamba kazi ya Mungu inakaribia mwisho wake. Kuangalia chini kutoka angani ni sawa na kutazama kwa mara nyingine mandhari ya kuchosha ya matawi yaliyonyauka na majani yaliyoanguka, ya mashapo yaliyopeperushwa kwa upepo wa majira ya kupukutika kwa majani, inaonekana kama ufunuo unakaribia kutokea miongoni mwa wanadamu, kama kwamba yote yanakaribia kugeuzwa kuwa ukiwa. Labda ni kwa sababu ya kiwango cha hisi cha Roho, ndio daima huwa kuna hali ya kutokuwa na furaha ndani ya moyo, na kipande cha faraja tulivu, lakini hii pia imechanganywa na kaisi fulani cha huzuni. Huu unaweza kuwa ufafanuzi wa maneno ya Mungu kwamba “mwanadamu anaamka, kila kitu kilicho duniani kiko katika utaratibu, na siku za kunusurika kwa dunia hazipo tena, kwa maana Mimi Nimefika!” Watu wanaweza kuwa hasi kwa kiasi fulani baada ya kuyasikia maneno haya, au wanaweza kusikitishwa kidogo na kazi ya Mungu, au wanaweza kuzingatia sana hisia iliyo katika roho zao. Lakini kabla ya kukamilisha kazi Yake duniani, Mungu hangeweza kuwa mpumbavu kiasi hicho kuwapa watu uwongo kama huo. Ikiwa kweli una hisia kama hizo, basi inaonyesha wewe huzingatia sana hisia zako, kwamba wewe ni mtu ambaye hufanya upendavyo, na humpendi Mungu; inaonyesha kwamba watu kama hao huzingatia sana mambo ya miujiza, na hawamsikilizi Mungu kabisa. Kwa sababu ya mkono wa Mungu, haijalishi jinsi watu wanavyojaribu kuondoka, hawawezi kuiepuka hali hii. Ni nani anayeweza kuuiepuka mkono wa Mungu? Ni wakati gani ambapo hadhi na hali yako havikupangwa na Mungu? Kama unateseka au umebarikiwa, ungewezaje kujikwapua kutoka kwa mkono wa Mungu? Hili si suala la

kibinadamu, ni hitaji la Mungu kabisa—nani asingetii kwa sababu ya hili?

“Mimi nitatumia kuadibu ili kueneza kazi Yangu katika Mataifa, ambayo ni kusema, Nitatumia nguvu dhidi ya wale wote walio watu wa Mataifa. Kwa kawaida, kazi hii itafanyika kwa wakati mmoja na ile kazi Yangu miongoni mwa wale waliochaguliwa.” Kwa kutamka maneno haya, Mungu anaanza kazi hii kote kote ulimwenguni, nayo ni hatua ya kazi ya Mungu, ambayo tayari imeendelea kufikia kiwango hiki; hakuna mtu anayeweza kugeuza mambo kuwa bora. Msiba utashughulikia sehemu moja ya wanadamu, na kuwasababisha kuangamia pamoja na ulimwengu. Wakati ulimwengu unaadibiwa rasmi, Mungu huonekana rasmi kwa watu wote. Na kwa sababu ya kuonekana Kwake, watu wanaadibiwa. Zaidi ya hayo, Mungu alisema pia, “Wakati Ninafungua rasmi hati ya kukunjwa ndio wakati watu ulimwenguni kote wanaadibiwa, wakati watu wote duniani wanakabiliwa na majaribu.” Kutokana na hili inaweza kuonekana wazi kwamba maudhui ya mihuri saba ni maudhui ya kuadibu, ambako ni kusema, kuna msiba katika mihuri saba. Hivyo, leo, mihuri saba bado haijafunguliwa; “majaribio” yanayotajwa hapa ni kuadibu ambako mwanadamu anapitia, na kati ya kuadibu huku kundi la watu litapatwa ambalo litakubali rasmi “cheti” kinachotolewa na Mungu, na hivyo watakuwa watu katika ufalme wa Mungu. Hizi ni asili za wana na watu wa Mungu, na leo bado hazijaamuliwa, na zinaweka tu msingi kwa ajili ya uzoefu wa baadaye. Ikiwa mtu ana uzima wa kweli, ataweza kusimama imara wakati wa majaribio, na ikiwa hana uzima, basi hii inathibitisha kwa hakika kwamba kazi ya Mungu haijakuwa na athari kwake, kwamba yeye hujaribu kupata faida kutokana na machafuko, na hazingatii maneno ya Mungu. Kwa sababu hii ni kazi ya siku za mwisho, ambayo ni kuikamilisha enzi hii badala ya kuendelea na kazi, kwa hiyo Mungu anasema, “Kwa maneno mengine, ni maisha ambayo mwanadamu hajawahi kupitia kutoka wakati wa uumbaji mpaka siku ya leo, na hivyo Ninasema kwamba Ninafanya kazi ambayo haijawahi kufanyika mbeleni,” na pia Anasema, “Kwa sababu siku Yangu inakaribia kwa wanadamu wote, kwa sababu haionekani kuwa mbali, lakini iko mbele ya macho ya mwanadamu.” Katika nyakati zilizopita, Mungu Mwenyewe aliangamiza miji kadhaa, lakini hakuna hata mmoja kati ya miji hiyo ulioteketewa sawa na wakati wa mwisho. Ingawa, katika siku zilizopita, Mungu aliangamiza Sodoma, Sodoma ya leo haipaswi kutendewa kama nyakati zilizopita—haipaswi kuangamizwa moja kwa moja, bali kushindwa kwanza na kisha kuhukumiwa, na hatimaye, kupitia adhabu ya milele. Hizi ndizo hatua za kazi, na mwishowe, Sodoma ya leo itateketewa katika mfuatano sawa na maangamizo ya ulimwengu ya wakati uliopita—ambao ni mpango wa Mungu. Siku ambayo Mungu ataonekana ndiyo siku ya shutuma rasmi, na sio kuiokoa kwa njia ya kuonekana Kwake. Hivyo, Mungu anasema, “Mimi huonekana kwa ufalme mtakatifu, na kujificha kutoka kwa nchi ya uchafu.” Kwa sababu Sodoma ya leo ni chafu, Mungu haionekani kwayo kwa hakika, lakini Anatumia njia hii kuiadibu—hujaona jambo hili wazi? Inaweza kusemwa kwamba

hakuna mtu duniani anayeweza kuuona uso halisi wa Mungu. Mungu hajawahi kuonekana kwa mwanadamu, na hakuna mtu anayejua Mungu yuko katika kiwango gani cha mbinguni. Hili ndilo limewasababisha watu wa leo kuwa katika hali hii. Kama wangeuona uso wa Mungu, huo hakika ungekuwa wakati ambao mwisho wao ungefichuliwa, wakati ambapo kila mmoja anaainishwa kulingana na aina. Leo, maneno katika uungu yanaonyeshwa moja kwa moja kwa watu, ambalo linatabiri kwamba siku za mwisho za wanadamu zimewadia, na hazitakaa muda mrefu zaidi. Hii ni mojawapo ya ishara za watu kutiishwa kwa majaribio wakati ambapo Mungu anaonekana kwa watu wote. Hivyo, ingawa watu hufurahia maneno ya Mungu, daima wao huwa na hisia ya kuogofya, kama kwamba msiba mkubwa unakaribia kuwafika. Watu wa leo ni kama jurawa katika nchi zenye barafu, ambao ni kama kwamba kifo kinawalazimishia ulipaji wa deni na kuwaacha bila njia yoyote ya kuishi. Kwa sababu ya deni la kifo ambalo mwanadamu anadaiwa, watu wote wanahisi kuwa siku zao za mwisho zimewadia. Hiki ndicho kinachofanyika katika mioyo ya watu duniani kote, na ingawa hakifichuliwi kwa nyuso zao, kile kilicho ndani ya mioyo yao hakiwezi kujificha kutoka kwa macho Yangu—huu ni uhalisi wa mwanadamu. Pengine, mengi ya maneno yanachaguliwa vibaya kwa kiasi fulani—lakini ni maneno yaya haya ambayo yanafaa kuonyesha tatizo. Kila mojawapo ya maneno yanayonenwa kutoka kinywani mwa Mungu yatatimizwa, kama ni ya zamani au ya sasa; yatafanya ukweli uonekane mbele ya watu, karamu kwa macho yao, wakati ambao watakanganywa na kuchanganyikiwa. Je, bado hujaona wazi leo ni enzi gani?

Sura ya 30

Watu wengine wanaweza kuwa na utambuzi kidogo katika maneno ya Mungu, lakini hakuna yeyote kati yao ambaye huamini hisia zake; wao huogopa sana kuingia katika ukanaji. Hivyo, wao kila mara wamegeuka kati ya furaha na huzuni. Ni haki kusema kwamba maisha ya watu wote yamejaa huzuni; kusongeza hili katika hatua nyingine zaidi, kuna usafishaji katika maisha ya kila siku ya watu wote, lakini Naweza kusema kwamba hakuna anayepata ufunguliwaji wowote katika roho yake kila siku, na ni kana kwamba milima mitatu mikuu inakilemea kichwa chake. Hakuna maisha yao yoyote yaliyo na furaha na shangwe kila wakati—na hata wakati ambapo wana furaha kidogo, wao wanajaribu tukujifanya kuwa wana furaha. Ndani ya mioyo yao, watu kila mara huwa na hisi ya kitu fulani kisichokwisha. Hivyo, hawako thabiti ndani ya mioyo yao; maishani, mambo huonekana kuwa matupu na yasiyo haki, na inapohusu kumwamini Mungu, wao wana shughuli nyingi na wanapungukiwa na wakati, ama sivyo watakosa wakati wa kula na kunywa maneno ya Mungu, au hawajui jinsi ya kula na kunywa maneno ya Mungu ipasavyo. Hakuna hata mmoja kati yao aliye na amani, na mwenye akili timamu, na thabiti ndani ya moyo wake. Ni kana kwamba daima wameishi chini ya anga lililotanda mawingu, kana kwamba wao huishi katika anga isiyo na hewa safi, na hili

limesababisha kuchanganyikiwa katika maisha yao. Mungu daima hunena kuelekea udhaifu wa watu moja kwa moja, Yeye daima huwagonga katika udhaifu wao—hamjaona kwa dhahiri toni ambayo kwayo Amenena kote? Mungu kamwe hajawahi kuwapa watu nafasi ya kutubu, na Yeye huwafanya watu waishi katika “mwezi” bila hewa safi. Tangu mwanzo mpaka leo, kwa nje, maneno ya Mungu yamefichua asili ya mwanadamu, lakini hakuna anayeweza kuona kwa dhahiri kiini cha maneno haya. Inaonekana kwamba kwa kufichua asili ya mwanadamu, watu huja kujijua na hivyo huja kumjua Mungu, lakini hii si njia katika kiini. Toni na kina kikuu zaidi cha maneno ya Mungu huonyesha tofauti wazi kati ya Mungu na mwanadamu. Katika hisia zao, jambo hili huwafanya watu kuamini bila kufahamu kwamba Mungu ni asiyeifikika na asiyeingilika; Mungu huleta kila kitu hadharani, na inaonekana kwamba hakuna anayeweza kurudisha uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu kwa namna ulivyokuwa. Si vigumu kuona kwamba lengo la matamshi yote ya Mungu ni kutumia maneno kuwapindua watu wote, na hivyo kutimiza kazi Yake. Hizi ndizo hatua za kazi ya Mungu. Lakini hiki sicho kile ambacho watu huamini katika mawazo yao. Wao huamini kwamba kazi ya Mungu inakaribia kilele chake, kwamba inakaribia athari yake ya kutambulika sana ili kushinda joka kuu jekundu, ambalo ni kusema, kuyafanya makanisa yasitawi, na hakuna anayekuwa na dhana kuhusu Mungu mwenye mwili, ama sivyo watu wote kumjua Mungu. Lakini hebu tusome kile ambacho Mungu anasema: “Katika mawazo ya watu, Mungu ni Mungu, na hawezi kushughulishwa kwa urahisi, ihali mwanadamu ni mwanadamu, na hapaswi kuwa mpotovu kwa urahisi ... na kutokana na hili, wao kila mara huwa wanyenyekevu na wavumilivu mbele Yangu; hawana uwezo wa kutangamana na Mimi, kwani wana dhana nyingi sana.” Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba, haijalishi kile asemacho Mungu au kile afanyacho mwanadamu, watu hawawezi kabisa kumjua Mungu; kwa sababu ya nafasi inayochukuliwa na kiini chao, lolote litokealo, wao, mwishowe, hawawezi kumjua Mungu. Hivyo, kazi ya Mungu itaisha wakati ambapo watu watajiona kama wana wa jehanamu. Hakuna haja ya Mungu kuachia huru ghadhabu Yake kwa watu, au kuwashutumu moja kwa moja, au hatimaye kuwahukumu kifo ili kuhitimisha usimamizi Wake wote. Yeye hupiga soga tu kwa mwendo Wake mwenyewe, kana kwamba ukamilishaji wa kazi Yake ni wa ziada, kitu fulani kinachotimizwa kwa wakati Wake wa ziada bila juhudi hata kidogo. Kutoka nje, inaonekana kuna haraka fulani kwa kazi ya Mungu—lakini Mungu hajafanya chochote, Yeye hafanyi chochote ila kunena. Kazi miongoni mwa makanisa siyo ya kiwango kikubwa kama ya nyakati zilizopita: Mungu hawaongezi watu, au kuwafukuza, au kuwafichua—kazi kama hiyo ni ya upuuzi sana. Inaonekana kama kwamba Mungu hafikirii kufanya kazi kama hiyo. Yeye husema tu kidogo ya kile Anachopaswa kusema, baadaye Yeye hugeuka na kutoweka bila kuonekana—ambalo, kwa kawaida, ni onyesho la kukamilika kwa matamshi Yake. Na kipindi hiki kitakapofika, watu wote wataamka kutoka katika usingizi wao. Mwanadamu amekuwa kwa usingizi wa uchovu kwa maelfu ya miaka, wamekuwa katika usingizi kabisa. Na

kwa miaka mingi, watu wamekuwa wakikimbia huku na kule katika ndoto zao, na hata wao hulia katika ndoto zao, wasiweze kuzungumza kuhusu udhalimu ulio ndani ya mioyo yao. Hivyo, wao “huhisi huzuni kidogo ndani ya mioyo yao”—lakini watakapoamka, watagundua ukweli wa kweli, na kutamka ghafula kwa mshangao: “Kwa hiyo hiki ndicho kinachoendelea!” Hivyo inasemekana kwamba, “Leo, watu wengi sana bado wamelala fofofu. Ni wakati tu ambapo wimbo wa ufalme husikika ndipo wao hufumbua macho yao yenye usingizi na kuhisi huzuni kidogo ndani ya mioyo yao.”

Hakuna roho ya yeyote ambayo imewahi kufanywa huru, kamwe roho ya mtu yeyote haijawahi kuwa changamfu na yenye furaha. Wakati ambapo kazi ya Mungu itamalizika kabisa, roho za watu zitafanywa huru, kwani kila mmoja atakuwa amesainishwa kufuatana na aina, na hivyo wote watakuwa thabiti katika mioyo yao. Ni kana kwamba watu wako katika safari ya baharini iliyoenea sana na mioyo yao huwa thabiti wanaporudi nyumbani. Wafikapo nyumbani, watu hawatahisi tena kwamba dunia ni tupu na isiyo haki, lakini wataishi kwa amani katika nyumba zao. Hiyo ndiyo itakuwa hali miongoni mwa wanadamu wote. Hivyo, Mungu anasema kuwa watu “hawajawahi kamwe kuweza kujinasua kutoka kwa utumwa wa Shetani.” Hakuna anayeweza kujinasua kutoka katika hali hii huku akiwa katika mwili. Kwa sasa, hebu tuweke kando kile Mungu anasema kuhusu hali halisi mbalimbali za mtu, na tuzungumze tu juu ya siri ambazo Mungu bado hajamfunulia mwanadamu. “Mara nyingi mno watu wamenitazama Mimi na macho ya kudhihaki, kana kwamba mwili Wangu umefunikwa kwa miiba na ni wa kuchukiza sana kwao, na hivyo watu hunichukia Mimi sana, na huamini kwamba Sina thamani.” Kwa namna nyingine, kwa kiini, tabia halisi ya mwanadamu hufichuliwa katika maneno ya Mungu: Amefunikwa na manyoya, hakuna kinachopendeza kumhusu yeye, na hivyo chuki ya Mungu kwa mwanadamu huongezeka, maana mwanadamu ni nungunungu aliyejawa miiba tu asiye na chochote cha kupendeza. Kwa juujuu, maneno haya yanaonekana kufafanua fikira za mtu kwa Mungu—lakini kwa kweli, Mungu anachora picha ya mwanadamu kulingana na “mfano” wake. Maneno haya ni jinsi Mungu anavyoeleza kinananaga kuhusu mwanadamu, na ni kama kwamba Mungu amenyunyizia dawa ya kutengeneza filamu juu ya mfano wa mwanadamu; hivyo, mfano wa mwanadamu unajulikana sana kote ulimwenguni, na hata huwashangaza watu. Tangu wakati ambapo Alianza kunena, Mungu amekuwa akipanga majeshi Yake kwa vita vikubwa na mwanadamu. Yeye ni kama profesa wa aljebra wa chuo kikuu anayeweka wazi ukweli kwa mwanadamu, na kile kinachothibitishwa na ukweli Anaorodhesha—ushahidi na ushahidi wa kukabili—huwafanya watu wote washawishike kabisa. Hili ndilo kusudi la maneno yote ya Mungu, na ni kwa sababu ya hili ndio Mungu kwa kawaida huyatupa maneno haya ya siri kwa mwanadamu. “Mimi, kwa kifupi, Sina thamani kabisa moyoni mwa mwanadamu, Mimi ni kitu cha nyumba kisicho cha muhimu.” Baada ya kusoma maneno haya, watu hawana budi ila

kutamka ombi ndani ya mioyo yao, na wao huja kujua hali yao ya kuwa wadeni kwa Mungu, ambalo huwafanya wajishutumu, huwafanya kuamini kuwa mtu anapaswa kufa, na hana thamani hata kidogo. Mungu anasema, “ni kwa sababu ya jambo hili ndio Najikuta katika hali Niliyo ndani leo,” ambayo, inapounganishwa na hali halisi ya leo, huwafanya watu kujishutumu. Je, huu si ukweli? Iwapo ungefanywa kujijua, je, maneno kama “Napaswa kweli kufa!” yangetoka kinywani mwako? Hizo ndizo hali za kweli za mwanadamu, na hili halifai kufikiriwa sana—ni mfano tu unaofaa.

Kwa maana moja, Mungu anapoomba msamaha na uvumilivu kwa mwanadamu, watu huona kuwa Mungu anawafanyia mzaha, na kwa maana nyingine, wao pia huona uasi wao wenyewe—wanangojea tu Mungu ajitahidi Mwenyewe iwezekanavyo kwa mwanadamu. Zaidi ya hayo, tukizungumzia fikira za watu, Mungu anasema Yeye si hodari katika falsafa ya mwanadamu ya kuishi. Hivyo, kwa namna moja hili huwafanya watu kufananisha maneno haya kwa Mungu wa vitendo, na kwa namna nyingine, wao huona nia ya Mungu katika maneno Yake—Mungu anawadhihaki, kwa maana wanaelewa kuwa Mungu anafichua sura ya kweli ya mwanadamu, na Hawaambii watu kwa kweli kuhusu hali za kweli za Mungu. Maana ya asili ya maneno ya Mungu imejawa na dhihaka, mzaha, kicheko, na chuki kwa mwanadamu. Ni kana kwamba, katika kila analolifanya, mwanadamu anaipotosha sheria na kuchukua rushwa; watu ni makahaba, na Mungu anapofungua kinywa Chake kunena, wao hutetemeka kwa hofu, wakihofu kabisa kuwa ukweli kuwahusu utafichuliwa kwelikweli, ukiwaacha na aibu kuu wasiweze kumtazama yeyote. Lakini ukweli ni ukweli. Mungu haachi matamshi Yake kwa ajili ya “toba” ya mwanadamu; kadri watu wanavyoona haya na aibu isiyoweza kuelezeka kwa maneno, ndivyo Mungu huimarisha kukazia macho Kwake kwa kuchoma juu ya nyuso zao. Maneno kutoka kwa kinywa Chake huyaweka wazi matendo yote mabaya ya mwanadamu—huku tu ndiko kuwa na haki na bila upendeleo, hii tu ndiyo inaitwa Qingtian,^[a] hii tu ndiyo hukumu kutoka kwa mahakama kuu zaidi ya watu. Hivyo, wakati ambapo watu wanasoma maneno ya Mungu, wao wanakumbwa ghafla na mshtuko wa moyo, shinikizo lao la damu hupanda, ni kana kwamba wanaugua ugonjwa wa moyo, ni kana kwamba utokaji wa damu ya ubongo unataka kuwarudisha katika paradiso ya magharibi kukutana na mababu zao—huu ndio mjibizo wao wanaposoma maneno ya Mungu. Mwandamu anafanywa dhaifu kwa miaka mingi ya kazi ngumu, yeye ni mgonjwa ndani na nje, kila sehemu yake inaugua, kutoka moyoni mwake hadi kwa mishipa yake ya damu, utumbo mpana, uchango, tumbo, mapafu, figo, na kadhalika. Hakuna chochote katika mwili wake wote kilicho na afya. Hivyo, kazi ya Mungu haifiki kiwango ambacho mwanadamu hawezi kukifikia, lakini huwasababisha watu kujijua. Kwa sababu mwili wa mwanadamu umezungukwa na kushambuliwa na virusi, na kwa sababu amekuwa mzee, siku ya kifo chake hukaribia, na hakuna namna ya kurudi nyuma. Lakini hii ni sehemu tu ya hadithi; maana ya

ndani bado haijafichuliwa, kwa kuwa asili ya ugonjwa wa mwanadamu inatafutwa. Kwa kweli, wakati ambao ukamilifu wa kazi ya Mungu unakamilishwa sio wakati ambao kazi Yake duniani inakamilika, kwa maana mara tu hatua hii ya kazi inapokamilika, hakutakuwa na njia ya kutekeleza ile kazi ya wakati ujao katika mwili, na Roho wa Mungu atahitajika kuikamilisha. Hivyo, Mungu anasema, “Wakati ambapo Mimi ninafungua rasmi kitabu ndipo watu kote ulimwenguni wanaadibiwa, wakati ambapo kazi Yangu hufika kilele chake, wakati ambapo watu kote duniani wanapitia majaribio.” Wakati ambapo kazi katika mwili inaisha sio wakati ambapo kazi ya Mungu hufikia kilele chake—kilele cha wakati huu kinahusu tu kazi wakati wa hatua hii, na sio kilele cha mpango wote wa usimamizi. Hivyo, mahitaji ya Mungu kwa mwanadamu si ya juu. Yeye anauliza tu watu wajijue, hivyo kutumikia hatua ifuatayo ya kazi, ambayo kwayo mapenzi ya Mungu yatakuwa yametimizwa. Kadri kazi ya Mungu inavyobadilika, ndivyo “kitengo cha kazi” cha watu kinavyobadilika. Leo ni hatua ya kazi ya Mungu duniani, na hivyo lazima wafanye kazi kule mashinani. Katika wakati ujao, itakuwa lazima kusimamia taifa, na hivyo watatumwa katika Kamati ya Kati. Wakienda kutembea ng’ambo, itawabidi washughulikia taratibu za kwenda nchi za kigeni. Katika nyakati hizo watakuwa katika nchi za kigeni, mbali kutoka kwa nchi yao—lakini hii hata hivyo itakuwa kwa ajili ya mahitaji ya kazi ya Mungu. Kama watu walivyosema, “Tutayatoa maisha yetu kwa Mungu ikibidi”—je, hii siyo njia ambayo itatemelewa katika siku za usoni? Ni nani amewahi kufurahia maisha kama hayo? Mtu anaweza kusafiri kote, atembelee nchi za kigeni, apaceane mwongozo kule mashambani, ajifanye mwenyeji miongoni mwa watu wa kawaida, na anaweza pia kuzungumza juu ya maswala muhimu ya taifa na wanachama wa mashirika ya ngazi za juu; na ikibidi, anaweza binafsi kuonja maisha katika jahanamu, kisha baadaye anaweza kurudi na bado aweze kufurahia baraka za mbinguni—je, hizi si baraka za mwanadamu? Ni nani amewahi kufananishwa na Mungu? Ni nani amewahi kusafiri katika mataifa yote? Kwa kweli, watu wangeweza kuelewa kidogo juu ya baadhi ya maneno ya Mungu bila ishara wala maelezo—ni kwamba tu hawajiamini, ndiyo ambayo imeipanua kazi ya Mungu mpaka leo. Kwa sababu watu hukosa mengi sana—kama Mungu alivyosema, “hawana chochote”—kazi ya leo husababisha matatizo makubwa mno kwao; na zaidi, udhaifu wao, kwa kawaida, umekizuia kinywa cha Mungu—na je, vitu hivi sivyo hasa vinavyoizuia kazi ya Mungu? Je, bado huwezi kuona hili? Kuna maana fiche katika yote asemayo Mungu. Mungu anaponena, Yeye hufahamu vizuri suala lililoko mbele yake na kulitumia ipasavyo, na kama hekaya, maneno yote Anenayo huwa na ujumbe wa kina. Maneno haya rahisi yana ujumbe wa kina, na hivyo huelezea maswala muhimu—je, hili silo ambalo maneno ya Mungu ni bora kwalo? Je, unajua hili?

Tanbihi:

a. Qingtian: Neno hili limetumika kutaja hakimu mwenye haki wakati wa kifalme wa China.

Sura ya 31

Tabia ya Mungu hujumuishwa katika matamko yote ya Mungu, lakini wazo kuu la maneno Yake ni kufichua uasi wa wanadamu wote na kufunua mambo kama kutotii, kuasi, utovu wa haki, udhalimu, na kutoweza kumpenda Mungu kweli. Ni kiasi kwamba, maneno ya Mungu yamefikia kiwango ambacho Yeye husema kwamba kila kinyweleo katika miili ya watu kina upingaji kwa Mungu, kwamba hata kapilari zao zina ukinzani kwa Mungu. Ikiwa watu hawatajaribu kuchunguza hili, wao daima watakuwa wasioweza kuyajua, na hawataweza kamwe kuyaweka kando. Ambayo ni kusema, virusi vya upingaji wa Mungu vitaenea ndani yao na hatimaye, itakuwa kana kwamba seli zao nyeupe za damu zimezila seli zao nyekundu za damu, zikiacha mwili wao wote bila seli nyekundu za damu; mwishowe, watakufa kutokana na lukemia. Hii ndiyo hali halisi ya mtu, na hakuna yeyote anayeweza kuikana. Kwa kuzaliwa kwenye eneo ambamo joka kuu jekundu hulala likiwa limejikunja, kuna angalau kitu kimoja ndani yaa kila mtu kinachoonyesha na ni mfano wa sumu ya joka kuu jekundu. Hivyo, katika hatua hii ya kazi, wazo kuu katika maneno yote ya Mungu limekuwa ni kujijua mwenyewe, kujikana mwenyewe, kujiacha mwenyewe, na kujiua mwenyewe. Yaweza kusemwa kuwa hii ni kazi ya msingi ya Mungu katika siku za mwisho, na kuwa duru hii ya kazi ndiyo pana zaidi na kamilifu kupita zote—ambayo inaonyesha kuwa Mungu anapanga kuhitimisha hii. Hakuna yeyote aliyetarajia hili, lakini pia ni kitu ambacho wamekitarajia katika hisi zao. Ijapokuwa Mungu hakusema hivyo kwa wazi sana, hisi za watu ni kali sana—wao daima huhisi muda ni mfupi. Naweza kusema kuwa kadri mtu anavyohisi hivi, ndivyo anavyokuwa na ufahamu wazi zaidi wa enzi. Si kwa kuona ulimwengu kama kawaida na hivyo kuyapinga maneno ya Mungu; bali, ni kujua maudhui ya kazi ya Mungu kupitia kwa njia ambayo kwayo Mungu hufanya kazi. Hii inaamuliwa na sauti ya matamshi ya Mungu. Kuna siri kutokana na sauti na matamshi ya Mungu ambayo hakuna yeyote amegundua na pia hasa ni iliyo ngumu sana kwa watu kuingia ndani yake. Kiini cha kwa nini watu hawawezi kuelewa maneno ya Mungu ni kuwa bado hawajui sauti ambayo Mungu huzungumzia—na kama wataimudu siri hii, wataweza kuwa na ujuzi fulani wa maneno ya Mungu. Maneno ya Mungu daima yamefuata kanuni moja: kuwafanya watu kujua kuwa maneno ya Mungu ni kila kitu, na kutatua matatizo yote ya mwanadamu kupitia kwa maneno ya Mungu. Kwa mtazamo wa Roho, Mungu huweka wazi matendo Yake, kwa mtazamo wa mwanadamu, Anafunua dhana za watu, kwa mtazamo wa Roho, Anasema mwanadamu si mzingatifu wa mapenzi Yake, na kwa mtazamo wa mwanadamu, Anasema Ameonja ladha tamu, chachu, chungu, na mbaya ya uzoefu wa binadamu, na Anakuja katika upepo na kuenda na mvua, kwamba Amepitia mateso ya jamii, na Amepitia milima na mabonde ya maisha. Haya ni maneno yanayosemwa kutoka kwa mitazamo tofauti. Anaponena kwa watu wa Mungu, ni kama msimamizi wa nyumba akiwakaripia watumwa, au kama kichekesho kifupi; maneno Yake

huwaacha watu wameaibika, bila mahali pa kujificha kutokana na aibu, ni kana kwamba wamezuiliwa na mamlaka ya kikabaila ili kukiri chini ya mateso makali. Wakati Anapozungumza na watu wa Mungu, Mungu hazuiliki kama wanafunzi wa chuo kikuu wanaolalamika wakifichua kashfa ndani ya serikali kuu. Iwapo maneno yote ya Mungu yangekuwa yanadhihaki, yangekuwa magumu zaidi kwa watu kuyakubali; hivyo, maneno ambayo hunenwa na Mungu ni halisi, hayana maandishi ya kimaumbo kwa mtu, lakini yanaonyesha hali halisi ya mtu moja kwa moja—ambayo inaonyesha kwamba upendo wa Mungu kwa mwanadamu sio maneno tu, bali ni kweli. Ingawa watu huthamini uhalisi, hakuna kitu chochote halisi kuhusu upendo wao kwa Mungu. Hii ndiyo inayokosekana kwa mwanadamu. Ikiwa upendo wa watu kwa Mungu si wa kweli, basi ukamilifu wa kila kitu utakuwa mtupu na wa uongo, kana kwamba wote ungetoweka kwa ajili ya hili. Ikiwa upendo wao kwa Mungu unazidi ulimwengu wote, basi pia hali yao na utambulisho, na hata maneno haya, yatakuwa halisi, na sio tupu—unaona hili? Je, umeona matakwa ya Mungu kwa mwanadamu? Mtu hapaswi tu kufurahia baraka za cheo, lakini kuishi kwa kudhihirisha ukweli wa cheo. Hili ndilo Mungu anataka kutoka kwa watu wa Mungu, na kwa binadamu wote, na sio nadharia kubwa iliyo tupu.

Kwa nini Mungu anasema maneno ya aina hii: “kana kwamba yote Nifanyayo ni jaribio la kuwafurahisha, kutokana na hilo wao daima huchukizwa na matendo Yangu”? Je, unaweza kuzungumza juu ya maonyesho halisi ya mwanadamu kumchukia sana Mungu? Katika dhana za watu, mwanadamu na Mungu “wanapendana kwa shauku,” na leo, hamu ya watu kwa maneno ya Mungu imefikia kiwango cha kuwa wao hutamani kwa hamu kummeza Mungu kwa funda moja—lakini Mungu anasema aina ya maneno yafuatayo: “Mtu hunidharau Mimi. Kwa nini upendo wangu umelipwa na chuki ya mwanadamu?” Je, hii sio amana ya madini ndani ya watu? Je, hii sio inayopasa kuchimbuliwa? Hii ndiyo kasoro ya ukimbizaji wa watu, ni suala kubwa ambalo linapaswa kutatuliwa, na ni simba ambaye husimama kwa njia ya ujuzi wa mwanadamu juu ya Mungu na ambayo inapaswa kuondolewa kwa mwanadamu—je, hili sio linalopaswa kufanyika? Kwa sababu, kama nguruwe, mtu hana kumbukumbu, na daima hutamani raha, Mungu humpa mtu dawa ya usahaulifu—Anazungumza zaidi, anasema zaidi, na Anawakamata watu kwa masikio na kuwafanya wasikize kwa makini, na kuwavisha vifaa vya kusikizia. Kuhusu baadhi ya maneno Yake, kusema mara moja tu hakuwezi kutatua tatizo; yanapaswa kusemwa tena na tena, kwa maana “watu daima husumbuliwa na usahaulifu katika maisha yao, na siku za maisha ya wanadamu wote ziko katika mchafukoge.” Kwa njia hii, watu wanaweza kuokolewa kutoka kwa hali ambayo kwayo “wanasoma wakati wanapokuwa na wakati, wanasikiliza wakiwa hawana kazi, na kuyaacha wakati hawana muda; ikiwa maneno yanasemwa leo, wanayazingatia, lakini watayapuuza, ikiwa hayatasemwa kesho.” Kadri asili ya watu

inavyohusika, kama leo Mungu angezungumza juu ya hali yao ya kweli na wapate ujuzi wake kamili, basi wangejawa na majuto—lakini baadaye, wangerejelea njia zao za zamani, wakitahadhari maneno ya Mungu na kurudia yale hapo juu wakati wanapokumbushwa. Hivyo, wakati unapofanya kazi au kuzungumza, usisahau kiini hiki cha mwanadamu; ingekuwa ni kosa kutelekeza kiini hiki wakati wa kufanya kazi. Katika kufanya kazi yote, hasa ni muhimu kuzungumza kwa kuzingatia dhana za watu. Hasa, unapaswa kuongeza ufahamu wako mwenyewe kwa maneno ya Mungu na kuyawasilisha Hii ndiyo njia ya kuwapa watu na kuwaruhusu wajijue wenyewe. Katika kutoa kwa watu kwa kutegemea maudhui ya maneno ya Mungu, kwa hakika itawezekana kuelewa hali yao halisi. Katika maneno ya Mungu, inatosha kuelewa hali halisi ya mwanadamu na hivyo kuwapa—na kwa hivyo, Sitasema zaidi juu ya maneno ya Mungu kuonyesha kuwa “Mungu alikubali mwaliko wa kukaa katika meza ya karamu duniani.”

Sura ya 32

Maneno ya Mungu huwaacha watu wakikuna vichwa vyao; ni kana kwamba, Anapozungumza, Mungu anaepukana na mwanadamu na kuzungumza na hewa, kana kwamba Hafikirii hata kidogo kuzingatia zaidi matendo ya mwanadamu, na Hatilii maanani kabisa kimo cha mwanadamu, kana kwamba maneno Anayozungumza hayaelekezwi kwa dhana za watu, lakini kuepukana na mwanadamu, kama lilivyokuwa kusudi la Mungu la asili. Kwa sababu nyingi sana, maneno ya Mungu hayaeleweki na mwanadamu hawezi kuyapenya. Hili halishangazi. Lengo la asili la maneno yote ya Mungu si kwa watu kupata ujuzi au ustadi kwayo; badala yake, ni njia moja kati ya zile Mungu ametumia kufanya kazi kutoka mwanzo hadi leo. Bila shaka, kutoka kwa maneno ya Mungu watu wanapata vitu vinavyohusiana na mafumbo, ama vitu vinavyowahusu Petro, Paulo, na Ayubu—lakini hili ndilo wanalopaswa kufikia, na kile wanachoweza kufikia, na, kama ifaavyo kimo chao, hili tayari limefikia kilele chake. Mbona matokeo ambayo Mungu anauliza yafikiwe si ya juu, lakini Amezungumza maneno mengi sana? Hili linahusiana na kuadibu Anakozungumzia, na kwa kawaida, yote yanafanikishwa bila watu kutambua. Leo, watu wanastahimili mateso makuu zaidi chini ya mashambulio ya maneno ya Mungu. Kwa juu juu, hakuna kati yao anayeonekana kuwa ameshughulikiwa, watu wameanza kuwekwa huru katika kufanya kazi yao, na watendaji-huduma wamepandishwa cheo kuwa watu wa Mungu—na katika hili, inaonekana kwa watu kwamba wameingia katika raha. Kwa kweli, ukweli ni kwamba, kutoka kwa utakasaji, wote wameingia katika kuadibu kukali zaidi. Kama tu vile Mungu anavyosema, “Hatua za kazi Yangu zinaungana kwa karibu moja kwa ifuatayo, kila moja ikiwa juu zaidi kila mara.” Mungu amewainua watendaji-huduma kutoka kwa shimo na kiberiti, ambapo kuadibu ni kukali zaidi. Hivyo, wanapitia hata taabu zaidi, ambayo ni vigumu kuitoroka. Je, kuadibu kama huko si kukali zaidi? Baada ya kuingia katika eneo la juu zaidi, kwa

nini watu wanahisi huzuni badala ya furaha yoyote? Mbona inasemekana kwamba baada ya kuokolewa kutoka kwa mikono ya Shetani, wanakabidhiwa joka kuu jekundu? Unakumbuka Mungu aliposema, “Sehemu ya mwisho ya kazi inamalizika katika nyumba ya joka kuu jekundu”? Unakumbuka wakati Mungu alisema, “Taabu ya mwisho ni kuwa na ushuhuda mkubwa sana, wa nguvu kwa ajili ya Mungu mbele ya joka kuu jekundu”? Iwapo watu hawakabidhiwi joka kuu jekundu, wangewezaje kuwa na ushuhuda mbele yake? Nani amewahi kusema maneno kama “Nimemshinda ibilisi” baada ya kujiua? Kujiua baada ya kuuona mwili wake kuwa adui—umuhimu halisi wa hili uko wapi? Mbona Mungu alizungumza hivyo? “Siyaangalii makovu ya watu, lakini katika sehemu yao ambayo haina makovu, na kutokana na hili Napata uridhisho.” Kama Mungu angetaka wale wasio na makovu kuwa maonyesho Yake, kwa nini Amezungumza kwa subira na ari maneno mengi kutoka kwa mtazamo wa mwanadamu kulipiza kisasi dhidi ya dhana za watu? Mbona Ajisumbue na hilo? Mbona Ajitaabishe kufanya jambo kama hilo? Hivyo inaonyesha kwamba kuna umuhimu wa kweli kwa kupata mwili kwa Mungu, kwamba “hangefutilia mbali” mwili baada ya kupata mwili na kukamilisha kazi Yake. Mbona inasemekana kwamba “dhahabu haiwezi kuwa safi na mwanadamu hawezi kuwa mtimilifu”? Maneno haya yanaweza kuelezwa vipi? Mungu anapozungumza kuhusu kiini cha mwanadamu, maneno Yake yanamaanisha nini? Kwa macho ya mwanadamu, mwili unaonekana kutoweza chochote, au sivyo kupungukiwa sana. Kwa macho ya Mungu, hili si muhimu hata kidogo—ilhali kwa watu, ni suala kubwa mno. Ni kana kwamba hawawezi kabisa kutatua hili na lazima lishughulikiwe binafsi na sayari za juu.—je, hii si dhana ya watu? “Katika macho ya watu, Mimi ni ‘nyota ndogo’ tu ambayo imeshuka kutoka angani; nyota ndogo mbinguni, na ujaji Wangu duniani leo uliagizwa na Mungu. Kwa hiyo, watu wamebuni fasiri zaidi za maneno ‘Mimi’ na ‘Mungu,’” Kwa kuwa wanadamu wamekuwa bure, kwa nini Mungu hufichua dhana zao kutoka kwa mitazamo tofauti? Je, hii pia inaweza kuwa hekima ya Mungu? Maneno kama hayo si mzaha? Kama Mungu anavyosema, “Ingawa kuna mahali ambapo Nimeweka katika mioyo ya watu, hawahitaji kwamba Niishi hapo. Badala yake, wanamsubiri ‘Mtakatifu’ katika mioyo yao kuwasili ghafla. Kwa sababu utambulisho Wangu ni ‘duni’ sana, Sifikii mahitaji ya watu na hivyo Naondolewa na wao.” Kwa sababu makadirio ya watu ni ya “juu sana,” vitu vingi “hayawezi kutimizwa” kwa Mungu, jambo ambalo linamweka “katika ugumu.” Watu hawajui hata kidogo kwamba wanachouliza kutoka kwa Mungu kuweza ni dhana zao. Na hii si maana halisi ya “Mtu mwerevu anaweza kuwa mwathiriwa wa ustadi wake mwenyewe”? Hii kwa kweli ni hali ya “kuwa stadi kama kanuni, lakini wakati huu mpumbavu”! Katika kuhubiri kwenu, mnawaomba watu waachane na Mungu wa fikira zao, lakini Mungu wa fikira zenu ameondoka? Je, maneno ya Mungu kwamba “Madai ninayofanya kutoka kwa mwanadamu si makubwa hata kidogo” yanawezaje kufasiriwa? Si ya kuwafanya watu wawe hasi na wapotovu ila kuwapa ufahamu safi wa maneno ya Mungu—mnaelewa? Je, Mungu mwenye mwili kweli ni “‘Mimi’

ambaye ni mwenye majivuno” kama watu wanavyofikiria?

Ingawa kuna wale ambao wamesoma maneno yote yaliyonenwa na Mungu na wanaweza kuyatolea muhtasari wa jumla, nani anayeweza kuzungumzia lengo la msingi la Mungu ni nini? Hili ndilo mwanadamu anakosa. Bila kujali ni kwa mtazamo gani Mungu huzungumza, lengo Lake la jumla ni kuwafanya watu wamjue Mungu aliye katika mwili. Kama hakungekuwa na chochote kisicho cha uungu—kama chote Alichu nacho kingekuwa sifa za kiasili za Mungu mbinguni—basi hakungekuwa na haja ya Mungu kusema mengi sana. Inaweza kusemwa kwamba kile watu wanakosa hutumika kama nyenzo za asili ambazo zinapatana na maneno ya Mungu. Ambayo ni kusema, kile kinachodhihirishwa kwa mwanadamu ni usuli wa kile Mungu husema kuhusu dhana za watu, na hivyo, watu huhudumia matamshi ya Mungu. Kwa kawaida, hili linategemezwa kwa kile Mungu husema kuhusu dhana za watu—ni kwa njia hii tu ndio hili linaweza kusemwa kuwa mchanganyiko wa nadharia na uhalisi, hapo tu ndipo watu wanaweza kufanywa kwa ufanisi kuwa makini kuhusu kujijua. Ingekuwa faida gani kama Mungu katika mwili Angelingana na dhana za watu na Mungu pia Alimshuhudia? Ni hasa kwa sababu ya hili kwamba Mungu hufanya kazi kutoka kwa upande hasi, Akitumia dhana za watu kusisitiza nguvu Yake kuu. Je, hii si hekima ya Mungu? Yote ambayo Mungu hufanya kwa ajili ya kila mtu ni mazuri—hivyo mbona msisifu wakati huu? Kama mambo yangefika mahali fulani, au siku ije, je, wewe, kama Petro, ungeweza kutamka maombi kutoka ndani yako katikati ya majaribu? Iwapo tu, kama Petro, bado unaweza kumsifu Mungu wakati uko katika mikono ya Shetani ndipo kutakuwa na maana ya kweli ya “kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa Shetani, kuushinda mwili, na kumshinda Shetani.” Je, huu si ushuhuda halisi zaidi kwa Mungu? Hii tu ndiyo athari inayofanikishwa na “uungu kuja kutenda na Roho aliyezidishiwa nguvu mara saba Anayefanya kazi ndani ya mwanadamu,” na hivyo, pia, ndiyo athari inayofanikishwa na “Roho akitoka kwa mwili.” Je, matendo kama hayo si halisi? Ulikuwa na mazoea ya kuzingatia uhalisi, lakini una maarifa ya ukweli kuhusu uhalisi leo? “Madai ninayofanya kutoka kwa mwanadamu si makubwa hata kidogo, lakini watu wanaamini vinginevyo. Hivyo, ‘unyenyekavu’ wao unafichuliwa katika kila tendo lao. Daima wanastahili kutembea mbele Yangu wakiniongoza njia, wakiwa na hofu kubwa kwamba Nitapotea, wakiogopa kwamba Nitazurura katika misitu ya kale ndani ya milima. Kwa hiyo, watu daima wameniongoza mbele, wakiwa na hofu sana kwamba Nitaingia katika gereza la chini ya ardhi.” Maarifa yenu kuhusu maneno haya rahisi ni yapi—kwa kweli mnaweza kuelewa asili ya maneno ya Mungu ndani yao? Mmezingatia ni dhana gani zenu ambazo Mungu amezungumza maneno kama hayo kuzihusu? Je, kila siku uangalifu wenu uko kwa suala hili muhimu? Katika sentensi ya kwanza ya sehemu ifuatayo, ambayo inakuja baadaye kwa karibu, Mungu anasema, “Lakini watu hawajui mapenzi Yangu na wanaendelea kuombea vitu kutoka Kwangu, kana kwamba utajiri Niliowapa hauwezi kukidhi

mahitaji yao, kana kwamba mahitaji yanashinda ugavi.” Katika sentensi hii inaweza kuonekana dhana zilizo ndani zenu ni zipi. Mungu hakumbuki wala kuchunguza kile mlichofanya katika nyakati zilizopita, kwa hivyo msifikirie tena masuala ya nyuma. La muhimu zaidi ni kama mnaweza kuunda “roho ya Petro katika enzi ya mwisho” katika njia ya baadaye—je, mna imani ili kufikia hili? Kile Mungu huuliza kutoka kwa mwanadamu ni kumuiga Petro tu, kwamba watu waweze hatimaye kubuni njia ili kuliaibisha joka kuu jekundu. Ni kwa sababu ya hili ndio Mungu anasema, “Natumaini tu kwamba watu wana azimio la kushirikiana na Mimi. Siulizi kwamba wanipikie chakula kizuri, au wanipangie mahali pa kufaa ili Nilaze kichwa Changu...” Duniani, watu wanaulizwa wawe na “roho ya Lei Feng” katika miaka ya 1990 hadi 1999, lakini katika nyumba ya Mungu, Mungu anauliza kwamba mtengeneze “mtindo wa pekee wa Petro.” Je, mnaelewa mapenzi ya Mungu? Je, kweli mnaweza kujitahidi kwa ajili ya hili?

“Natembea juu ya ulimwengu, na Ninapotembea Ninaangalia kwa makini watu wa ulimwengu mzima. Kati ya umati wa watu duniani, hakujawahi kuwa na wowote ambao wanafaa kwa kazi Yangu ama ambao wananipenda kwa kweli. Hivyo, kwa wakati huu Ninahema kwa kuvunjika moyo, na watu wanatawanyika mara moja, wasikusanyike tena, wakiogopa sana kwamba ‘Nitawakamata wote katika wavu mmoja.’” Watu wengi sana, pengine, wanaona maneno haya kuwa magumu sana kuelewa. Wanauliza mbona Mungu haulizi mengi kutoka kwa mwanadamu, ilhali Yeye huhema kwa kuvunjika moyo kwa sababu hakuna wowote wanaofaa kwa ajili ya kazi Yake. Je, kuna ukinzani hapa? Kuzungumza neno kwa neno, kuna—lakini kwa uhalisi, hakuna ukinzani. Pengine bado unaweza kukumbuka Mungu aliposema, “Maneno Yangu yote yatakuwa na athari Ninayotaka sana.” Wakati Mungu anapofanya kazi katika mwili, watu hukazia macho kila tendo Lake kuona kile Atakachofanya hasa. Mungu anapotekeleza kazi Yake mpya kumwelekea Shetani katika ufalme wa kiroho, kunazo, kwa maneno mengine, dhana za aina yote zinazozalishwa miongoni mwa watu duniani kwa sababu ya Mungu katika mwili. Mungu ahemapo kwa kuvunjika moyo, yaani, Anapozungumza kuhusu dhana zote za mwanadamu, watu wanajaribu yote wawezayo kuzishughulika, na hata kuna wale ambao wanaamini hawana matumaini, kwa maana Mungu anasema kwamba wote ambao wana dhana kumhusu ni adui Zake—na basi watu wangewezaje kukosa “kutawanyika” kwa sababu ya hili? Hasa leo, wakati kuadibu kumefika, watu wanaogopa hata zaidi kwamba Mungu atawaondoa. Wanaamini kwamba baada ya wao kuadibiwa, Mungu “atawakamata wote katika wavu mmoja.” Ilhali ukweli si hivyo: Kama asemavyo Mungu, “Sitaki ‘kuwazuia’ watu katikati ya kuadibu Kwangu, wasitoroke kamwe. Kwa sababu usimamizi Wangu unakosa matendo ya mwanadamu, haiwezekani kumaliza kazi Yangu kwa ufanisi, jambo ambalo huizuia kazi Yangu kuendelea mbele kwa ufanisi.” Mapenzi ya Mungu si kwa kazi Yake kumalizika wakati watu wote wameuwawa—hiyo ingekuwa na faida gani? Kwa kufanya kazi ndani ya watu na kuwadibu,

Mungu kisha anaweka wazi matendo Yake kupitia kwao. Kwa sababu watu hawajawahi kuelewa kwamba tayari kuna kuadibu katika sauti ya maneno ya Mungu, hawajawahi kuwa na kuingia katika akili zao. Watu hawana uwezo wa kuonyesha uamuzi wao, na hivyo Mungu hawezi kusema chochote mbele ya Shetani, jambo ambalo linakomesha kazi ya Mungu kuendelea mbele. Hivyo Mungu anasema, “Wakati mmoja Nilimwalika mwanadamu kama mgeni katika nyumba Yangu, ilhali alikimbia huku na kule kwa sababu ya miito Yangu—kana kwamba, badala ya kumwalika kama mgeni, Nilikuwa Nimemleta eneo la maangamizi. Hivyo, nyumba Yangu iliachwa tupu, kwani mwanadamu daima aliepukana na Mimi na daima alikuwa akijihadhari dhidi Yangu. Hili liliniacha bila namna ya kutekeleza sehemu ya kazi Yangu.” Ni kwa sababu ya makosa ya mwanadamu katika kazi yake ndio Mungu anatoa mahitaji Yake ya mwanadamu kwa dhahiri. Na ni kwa sababu watu wanakosa kutimiza hatua hii ya kazi ndio Mungu anaongeza matamshi mengine—ambayo hasa ni “sehemu nyingine ya kazi kwa mwanadamu” ambayo Mungu huzungumzia. Lakini Sitazungumzia “kuwakamata wote katika wavu mmoja” ambayo Mungu anazungumzia, kwa sababu hili halihusiani sana na kazi ya leo. Kwa kawaida, katika “Maneno ya Mungu Kwa Ulimwengu Mzima,” maneno Yake mengi yanahusiana na mwanadamu—lakini watu wanapaswa kuelewa mapenzi ya Mungu; bila kujali kile Anachosema, makusudio Yake daima ni mazuri. Inaweza kusemwa kwamba kwa sababu njia ambazo Mungu hutumia kuzungumza ni nyingi sana, watu hawana uhakika kwa asilimia mia kuhusu maneno ya Mungu, na wanaamini kwamba mengi ya maneno ya Mungu yanazungumzwa kwa sababu ya vitu vya lazima vya kazi Yake, na hayana mengi ambayo ni ya kweli, jambo ambalo linawaacha wakiwa wamechanganyikiwa na kusumbuliwa na mawazo yao—kwani katika dhana zao, Mungu ni mwenye hekima sana, Hafikiwi na wao kabisa, ni kana kwamba hawajui chochote, na hawana habari kuhusu jinsi ya kula maneno ya Mungu. Watu hufanya maneno ya Mungu kuwa ya kuwazika tu na magumu kufahamika—kama asemavyo Mungu, “watu daima hutaka kuongeza ladha kwa matamshi Yangu.” Kwa sababu mawazo yao ni yenye utata sana, na “hufikiwa kwa shida” na Mungu, sehemu ya maneno ya Mungu yanazuiwa na mwanadamu, ikimwacha Yeye bila chaguo ila kuzungumza kwa namna ambayo ni waziwazi na dhahiri. Kwa sababu mahitaji ya watu ni “ya juu sana,” na kwa sababu fikira zao ni nyingi sana—kana kwamba wanaweza kuvuka na kuingia katika ufalme wa kiroho ili kuyaona matendo ya Shetani—hili limepunguza maneno ya Mungu, kwa maana kadiri anavyosema Mungu, ndivyo nyuso za watu zinavyokuwa za huzuni zaidi. Kwa nini hawawezi kutii tu, badala ya kutafakari mwisho wao? Iko wapi faida kwa hili?

Sura ya 33

Kwa ukweli, kutegemea kile ambacho Mungu amefanya ndani ya watu, na kuwapa, na vilevile kile ambacho watu wanacho, inaweza kusemwa kwamba matakwa Yake kwa watu sio

makubwa mno, kwamba hataki mengi kutoka kwao. Wangekosaje basi, kujaribu kumridhisha Mungu? Mungu humpa mwanadamu asilimia mia moja, lakini Huhitaji tu sehemu ndogo ya asilimia kutoka kwa watu—hii ni kuhitaji mengi sana? Je, Mungu analeta tatizo pasipo na chochote? Mara nyingi, watu huwa hawajijui, huwa hawajichunguzi mbele ya Mungu, na kwa hiyo huwa kuna nyakati nyingi ambapo wao hutegwa—hili lingefikiriwa vipi kuwa ni kushirikiana na Mungu? Iwapo kumewahi kuwa na wakati ambapo Mungu hakuweka mzigo mzito juu ya watu, wangevunjika kama udongo, na hawangekuwa na ari ya kutafuta vitu. Hivyo ndivyo walivyo watu, ama ni baridi au hasi, daima wasioweza kushirikiana na Mungu kwa utendaji, kila mara wao hutafuta sababu hasi ya kukubali kushindwa na wao wenyewe. Je, wewe kweli ni mtu anayefanya kila kitu sio kwa ajili yako mwenyewe, bali kumridhisha Mungu? Je, wewe kweli ni mtu asiyetegemea hisia, asiye na upendeleo wake mwenyewe, na ambaye anatimiza mahitaji ya kazi ya Mungu? “Kwa nini daima wao hujaribu kubishana na Mimi? Je, mimi ni msimamizi mkuu wa kituo cha biashara? Kwa nini Mimi hutimiza kwa moyo kamili kile ambacho watu hudai kutoka Kwangu, lakini Nitakacho kutoka kwa mwanadamu hakitimii?” Kwa nini Mungu huuliza mambo kama hayo mara kadhaa mfululizo? Kwa nini Analia kwa hofu hivyo? Mungu hajapata chochote kutoka kwa watu, yote aonayo ni kazi wanayochukua na kuchagua. Mbona Mungu asema, “lakini Nitakacho kutoka kwa mwanadamu hakitimii?” Jiulizeni: Tangu mwanzo hadi mwisho, ni nani awezaye kufanya kazi ya wajibu wake bila chaguo lolote? Ni nani asiyetenda kwa ajili ya hisia zilizo ndani ya moyo wake? Watu huzipa tabia zao uhuru, bila kuvumilia kwa yale wanayofanya, kana kwamba wanavua siku tatu na kuziacha nyavu zao nakushinda siku mbili bila kufanya chochote. Wao huwa moto na baridi kwa zamu: Wanapokuwa moto, wanaweza kuteketeza vitu vyote duniani, na wanapokuwa baridi, wanaweza kugandisha maji yote duniani. Hii si kazi ya mwanadamu, lakini ni analojia ya kufaa zaidi kuhusu hali ya mwanadamu. Huu si ukweli? Labda Nina “dhana” kuhusu watu, labda Ninawasingizia—lakini hata hivyo, “Ukiwa na ukweli utatembea ulimwengu mzima; bila ukweli, hutafika popote.” Ingawa hii ni methali ya binadamu, Nafikiri inafaa kutumiwa hapa. Sivunji mioyo ya watu kwa makusudi na kukanusha shughuli zao. Hebu Nishauriane nanyi kuhusu maswali fulani: Ni nani huchukulia kazi ya Mungu kama kazi ya wajibu wake mwenyewe? Ni nani aweza kusema, “Maadamu ninaweza kumridhisha Mungu, nitatoa yangu yote”? Ni nani awezaye kusema, “Bila kujali wengine, nitafanya yote ambayo Mungu anahitaji, na haijalishi kama kiasi cha kazi ya Mungu ni kirefu au kifupi, nitatimiza wajibu wangu; kufikisha kazi Yake mwisho ni shughuli ya Mungu, si kitu ninachofikiria”? Nani ana uwezo wa maarifa kama hayo? Haijalishi mnachofikiria—labda una ujuzi wa juu sana, kwa hivyo Nakubali, Nakubali kushindwa—lakini lazima Niwaambie kile ambacho Mungu anataka ni moyo mtiifu ulio mwaminifu na ulio na shauku, si moyo wa mbwa mwitu unaokosa shukrani. Unajua nini kuhusu “kujadiliana” huku? Tangu mwanzo hadi mwisho, “mmesafiri

ulimwenguni.” Wakati mmoja mko “Kunming,” na majira yake ya kuchipua daima, na kufumba na kufumbua mmewasili katika “Ncha ya Kusini” yenye baridi ya kukandamiza iliyofunikwa na theluji. Ni nani hajawahi kuvunja ahadi yake? Kile ambacho Mungu anataka ni roho ya, “Hakuna kupumzika mpaka kifo,” kile Anachotaka ni ile ambayo watu “hawarudi nyuma mpaka wafike ukuta wa kusini.” Kwa kawaida, kusudi la Mungu si kwa watu kufuata njia isiyo sahihi, bali kuwa na roho kama hiyo. Kama asemavyo Mungu, “Ninapolinganisha ‘zawadi’ walizotoa kwa vitu Vyangu, watu hutambua thamani Yangu mara moja, na wakati huo tu ndio wao huona kutopimika Kwangu.” Maneno haya yanaweza kuelezwa vipi? Labda, kusoma maneno yaliyo hapo kunakupa maarifa fulani, kwani Mungu hutoa moyo wote wa mwanadamu kwa uchunguzi, wakati huo watu huja kuyajua maneno haya. Lakini kwa ajili ya maana kubwa ya ndani ya maneno ya Mungu, watu bado hawaelewi mwili wa zamani, kwani hawajasoma katika chuo kikuu cha tiba, wala wao si wanaakiolojia, na kwa hiyo wanahisi kwamba neno hili jipya halifahamiki—na wakati huo tu ndipo wao husalimu amri kidogo. Kwa vile watu ni wadhaifu mbele ya mwili wa zamani; ingawa si kama mnyama mkali, wala kuweza kufutilia mbali wanadamu kama bomu la atomu, hawajui wafanye nini nao, kana kwamba wao ni wadhaifu. Lakini Kwangu, kuna njia za kushughulikia mwili wa zamani. Mwanadamu kukosa kamwe kufanya juhudi za kufikiri juu ya hatua ya kuzuia kumesababisha vioja mbalimbali vya mwanadamu kutokea ghafla siku zote mbele ya macho Yangu; kama tu alivyosema Mungu: “Nionyeshapo uzima Wangu kwao, wao hunitazama kwa macho yaliyokodoa, wakisimama mbele Yangu bila kujongea, kama nguzo ya chumvi. Na Ninapotazama kutokuwa kawaida kwao Mimi huwa na taabu kujizuia kucheka. Kwa sababu wananyosha mkono kuomba vitu kutoka Kwangu, Mimi huwapa vitu vilivyo mkononi Mwangu, nao huvikumbatia, wakivitunza kama mtoto aliyezaliwa hivi sasa, ishara waifanyayo tu mara moja.” Je, haya si matendo ya mwili wa zamani? Kwa vile, leo, watu wanaelewa, mbona wasiache, na badala yake bado wanaendelea? Kwa kweli, sehemu ya matakwa ya Mungu si yasiyofikiwa na mwanadamu, lakini watu hawayatilii maanani, kwa kuwa “Simwadibu mwanadamu kwa urahisi. Ni kwa sababu hii ndiyo watu daima wameipa miili yao uhuru. Hawafuati mapenzi Yangu, wamenirairai daima mbele ya kiti Changu cha hukumu.” Je, hiki si kimo cha mwanadamu? Si kwamba Mungu anatafuta makosa kwa makusudi, lakini kwamba huu ni uhalisi—ni lazima Mungu aeleze hili? Kama tu asemavyo Mungu, “Ni kwa kuwa ‘imani’ ya watu ni kubwa mno ndio wao ni ‘wa kusifiwa.’” Kwa sababu hii, Natii mipango ya Mungu, na kwa hiyo Sisemi mengi kuhusu hili; kwa sababu ya imani ya watu, Naelewa na kutumia hili, Nikitumia imani yao kuwafanya watekeleze kazi yao bila Mimi kuwakumbusha. Je, ni kosa kufanya hili? Je, hili silo hasa analohitaji Mungu? Labda, baada ya kusikia maneno kama haya, watu wengine huenda wakahisi kuchoshwa—kwa hivyo Nitanena kuhusu jambo lingine, ili kutowahukumu sana. Wakati ambapo wateule wote wa Mungu katika ulimwengu mzima watapitia kuadibu, na wakati ambapo hali ndani ya

mwanadamu itarekebisha, watu watafurahia kisirisiri ndani ya mioyo yao, kana kwamba wameepuka majonzi. Wakati huu, watu hawatajichagulia tena, kwani hili hasa ndilo tokeo lililotimizwa wakati wa kazi ya mwisho ya Mungu. Hatua Zake zikiwa zimeendelea mpaka leo, wana na watu wote wa Mungu wameingia katika kuadibu, na Waisraeli, pia, hawawezi kukwepa awamu hii, kwani watu wametiwa doa na uchafu ndani yao, na kwa hiyo Mungu anawaongoza watu wote kuingia katika tanuu kuu la kuyeyusha madini ili kusafishwa, ambayo ni njia ya lazima. Baada ya hili kupita, watu watafufuliwa kutoka kifo, ambalo hasa ndilo Mungu alitabiri katika “matamko ya Roho saba.” Sitanena zaidi kuhusu hili, ili Nisiwachokoze watu. Kwa vile kazi ya Mungu ni ya ajabu, unabii ulionenwa kutoka kinywani mwa Mungu lazima hatimaye utimizwe; Mungu anapowaambia watu wanene kuhusu dhana zao mara nyingine tena, wao huduwaa, na kwa hiyo mtu yeyote asiwe na wahaka au wasiwasi. Kama Nilivyosema tu, “Kuhusu kazi Yangu yote, kuliwahi kuwa na hatua iliyotekelezwa kwa mikono ya mwanadamu?” Je, unaelewa kiini cha maneno haya?

Sura ya 35

Siku hizi, binadamu wote, kwa viwango vinavyotofautiana, wameingia katika hali ya kuadibu. Kama tu alivyosema Mungu, “Naenda mbele na binadamu sako kwa bako.” Hii ni kweli kabisa, lakini watu bado hawawezi kulielewa kabisa wazo hili. Kutokana na hili, sehemu ya kazi ambayo wamefanya imekuwa si lazima. Mungu alisema, “Mimi husaidia na kuwaruzuku kwa mujibu wa kimo chao. Kwa kuwa wanadamu ndio wahusika wakuu wa mpango Wangu wote wa usimamizi, Ntoa ushauri zaidi kwa walio katika hii nafasi ya ‘binadamu’ ili waweze kuiigiza kwa moyo wote na kwa uwezo wao wote,” pamoja na, “Hata hivyo, Nakataa kukosoa dhamiri zao moja kwa moja; badala yake, Naendelea kuwaelekeza kwa uvumilivu na utaratibu. Hata hivyo, wanadamu ni dhaifu, na wasioweza kutekeleza kazi yoyote.” Kufikiri kwa Mungu ni huku: Hata Akiishia kuwaangamiza binadamu hawa wote, kazi Yake duniani bado itaendelea kwa mujibu wa mpango Wake wa asili. Mungu hafanyi kazi bure; kila kitu ambacho Yeye hufanya ni kizuri. Kama Petro alivyosema, “Hata Mungu angekuwa Anacheza na binadamu kana kwamba wao ni vitu vya kuchezea watoto, wanadamu wangepeweza kuwa na malalamiko yapi? Ni haki gani wangepeweza nayo?” Kwa siku ya sasa, je, hiki si kile ambacho Mungu anatumiza na binadamu? Wanadamu wanaweza kuwa na mtazamo huu kwa kweli? Kwa nini Petro wa miaka elfu kadhaa iliyopita aliweza kusema jambo kama hilo, ilhali “Petro” katika enzi ya leo yenye teknolojia ya hali ya juu, iliyofanywa kuwa ya kisasa hawawezi? Siwezi kusema kwa hakika kama historia inaendelea mbele au inarudi nyuma. Kama sayansi imechukua hatua kwenda mbele au kurudi nyuma, hadi sasa, bado ni swali ambalo hakuna anayeweza kulijibu. Kila kitu ambacho Mungu amefanya kwa binadamu kimekuwa kuwafanya wazuri na kuwakubalia kukua maishani. Je, watu hawawezi kulifahamu hili? Kila kitu kinachokufanya uwe mbaya ni kiwango

chako dhaifu; ni kiwango kikuu cha kuweza kudhuriwa, kilicho wazi kwa mashambulio ya Shetani. Je, unaelewa hili? Kwa nini Mungu alinena hivi? “Nawasihi kwa ukunjufu na uaminifu wote. Hawawezi kwa kweli kufanya Nilichowauliza?” Maneno haya yana maana gani? Kwa nini Mungu aliuliza swali hili? Linaonyesha kwamba kuna hali nyingi sana mbaya za binadamu, na aina moja tu ya hali mbaya inatosha kusababisha binadamu kujikwaa. Unaweza vilevile kutazama na uone kile ambacho kuendelea katika njia zako mbaya kitakuletea wewe. Yote ambayo Mungu hufanya huelekea kwa ukamilishaji wa binadamu. Je, hili linahitaji ufafanuzi wowote zaidi? Sidhani! Hoja inaweza kujengwa kwamba binadamu wamemilikiwa na Shetani, lakini ingekuwa bora zaidi kusema kwamba binadamu wamemilikiwa na ukanaji. Hii ni njia ambayo binadamu hujionyesha wenyewe; ni kiambatisho cha mwili wao. Kwa hivyo, wote wameingia katika ukanaji bila kufahamu, na pamoja na hilo, kuadibu. Huu ni mtego Mungu aliouandaa kwa binadamu, na ni huu wakati kwamba binadamu anapitia mateso kwa wingi. Kwa vile watu huishi katika ukanaji, ni vigumu wao kuachana na kuadibu. Je, hivi sivyo mambo yalivyo hasa siku hizi? Lakini binadamu wanawezaje kuyapuuza maneno ya Mungu: “Siku hizi, Shetani amekithiri kupita kiasi. Kwa nini Sichukui fursa hii kuringia kiini cha kazi Yangu ili kufichua nguvu Zangu?” Punde Nisemapo jambo fulani kuwakumbusha, watu kutoka makanisa huingia katika kuadibu mara moja. Hili ni kwa sababu baada ya miezi miwili ya kazi ya Mungu, watu bado hawapitii mbadiliko wowote wenye maana ndani. Wao huchambua tu maneno ya Mungu na mawazo yao wenyewe. Hata hivyo, katika ukweli halisi, hali zao hazijabadilika kabisa; wao bado ni wabaya. Hali ikiwa hii, Mungu anapotaja kwamba nyakati za kuadibu ziko karibu, watu huhuzunishwa sana, wakifikiria: “Mimi sijui kama nimejaaliwa na Mungu au la, wala sijui kama naweza kusimama imara chini ya kuadibu huku. Hata ni vigumu zaidi kujua ni mbinu gani ambazo Mungu atatumia kuwaadibu watu.” Binadamu wote wanatishwa na kuadibu, lakini hawawezi kubadilika. Wao huteseka tu kwa kimya, lakini pia wanaogopa kwamba hawataweza kusimama imara. Katika hali hiyo, bila adabu kutekelezwa kwao na bila mateso ya maneno, binadamu wote wameteleza katika kuadibu bila kufahamu. Hivyo, wote ni wenye wasiwasi na waliofadhaishwa. Hii inaitwa, “kuvuna walichopanda,” kwa kuwa binadamu hawaelewi kazi ya Mungu kabisa. Kwa kweli, Mungu hapendi kupoteza maneno yoyote zaidi kwa watu hawa; inaonekana Mungu amechukua njia tofauti ya kuwashughulikia ambayo si kuadibu halisi. Ni kama wakati ambapo mtu hushika kifaranga na kukiinua kuona ikiwa ni kuku jike au jogoo; hili huenda lisionekane kama jambo kubwa, lakini kifaranga mdogo atatishwa sana atang’ang’ana kuwa huru, kana kwamba anaogopa binadamu atamuua na kula nyama yake, kwa kuwa kifaranga hana ufahamu kujihusu. Mtu anawezaje kumuua na kumla kifaranga mwenye uzito wa aumsi chache tu. Huo haungekuwa upuuzi? Ni kama alivyosema Mungu kabisa: “Kwa nini, basi, watu huniepuka Mimi daima? Je, ni kwa sababu Nitawachukulia kama vifaranga wadogo, kuuawa punde washikwapo?” Kwa hivyo, mateso ya binadamu yote ni kujitolea “bila

ubinafsi,” na yanaweza kusemekana kuwa ni gharama bure kulipa. Ni kwa sababu hawajijui wenyewe ndiposa wao huhisi woga; kutokana na hilo, hawawezi kuweka maisha yao hatarini. Huu ni udhaifu wa binadamu. Je, maneno yanayonenwa na Mungu, “Mwishowe, acha binadamu wajijue wenyewe. Hili ni lengo Langu la mwisho,” yamepitwa na wakati? NI nani anajijua mwenyewe kwa kweli? Ikiwa mtu hajijui mwenyewe, basi ni nini kinachompa haki ya kuadibiwa? Chukua mfano wa wanakondoo. Wanawezaje kuchinjwa kama hawajakua kuwa kondoo? Mti ambao haujazaa matunda unawezaje kufurahiwa na binadamu? Kila mtu huchukulia “chanjo” kuwa za maana sana. Hivyo, watu wote wanafanya kazi ya kufunga, na kisha wanaona njaa. Huu ni mfano wa kuvuna walichopanda; wa kujiangamiza wao wenyewe, bali sio kutokana na ukatili wa Mungu au wa unyama. Ikiwa siku moja wanadamu watajijua wenyewe na kutetemeka kwa woga mbele ya Mungu, basi Mungu ataanza kuwaadibu. Ni kwa njia hii pekee ndiyo binadamu watakubali taabu kwa utii na kwa radhi. Na kuhusu leo je, hata hivyo? Watu wote hupokea kuadibu kinyume na hiari yao, kama watoto wanaolazimishwa kupika chakula. Hili likiwa hivyo, kwa nini wao wasijisikie raha? Kila mtu hufikiria, “Haidhuru! Maadamu ninaadibiwa, naweza vilevile kuinamisha kichwa changu na kukiri kosa! Nitafanyaje? Hata kama nalia, bado lazima nimridhishe Mungu, kwa hiyo nitafanyaje? Nani aliniambia nitembee moja kwa moja kwa njia hii? Haidhuru! Nitajichukulia kama asiye kuwa na bahati!” Hivi sivyo wanavyofikiria watu?

Kama alivyosema Mungu, “Kila mtu ana tabia nzuri, na hakuna anayethubutu kupinga. Wote wako chini ya uongozi Wangu, wakifanya kazi zao Nilizowapa.” Kwa dhahiri, hakuna binadamu hata mmoja hupokea kuadibu kwa radhi, na zaidi ya hayo, hili hutoka kwa Mungu, kwa sababu binadamu wote hutaka kuishi katika raha badala ya ghasia na vurugu. Mungu alisema, “Ni nani asiye na hofu ya kifo? Je, inawezekana watu kuhatarisha maisha yao?” Hii ni kweli kabisa; kila mtu huogopa kufa, isipokuwa, bila shaka, wakati ambapo ameliwa na hasira au kukata tamaa. Hiki ndicho kiini cha ubinadamu, na ni vigumu zaidi kusuluhisha. Leo Mungu amekuja hasa kusuluhisha mashaka haya. Binadamu wote ni wadhaifu, kwa hiyo Mungu amefanya kila juhudi kuja miongoni mwao kuanzisha hospitali ya kitaalam ili kuwatibu aina hii ya ugonjwa. Watu hawawezi kujinasua wenyewe kwa ugonjwa huu wa kutatiza, ndiyo kwa sababu wote hupata wasiwasi sana mpaka wakawa na uvimbe uchungu wa mdomo, na tumbo zao kupanuka. Baada ya muda wingi wa gesi waliyonayo hukua, na kusababisha ongezeko la shinikizo. Hatimaye, tumbo zao hupasuka na wote hufa. Kwa hivyo, wakati huo, Mungu ametibu haya maradhi mabaya ya binadamu, kwa sababu kila mtu amekufa. Je, huku si kutibu hali ya binadamu? Mungu kwa makusudi amekuja kuifanya kazi hii. Kwa sababu watu huogopa kifo kupita kiasi, Mungu Mwenyewe amekuja kushiriki kazi sawa na binadamu; kwa sababu wana ujasiri kidogo sana, Ameanza kwa kutoa maonyesho ya watu kutazama. Ni baada tu ya kuona

kitangulizi hiki ndipo mtu yeyote huwa radhi kutii. Kwa sababu hii, Mungu alisema, “Kwa kuwa hakuna mtu ambaye angeifanya kazi Yangu, Nimeingia vitani binafsi kukumbana na mapambano ya kufa na kupona dhidi ya Shetani.” Hivi ni vita vya kuamua mshindi na mshinde, kwa hiyo ama samaki wafe au wavu ukatike. Hili ni hakika. Kwa kuwa roho itashinda mwishowe, mwili lazima uwe shabaha ya kifo. Je, mnaelewa athari za hili? Hata hivyo, msiwe wepesi kuathirika kupita kiasi. Labda sentensi hii ni rahisi, au labda ni changamano. Hata hivyo, binadamu bado hawawezi kuielewa. Hili ni hakika. Binadamu wanaweza, kutokana na kuteseka kwao, kukubali usafishaji wa neno la Mungu; kisha mtu angeweza kusema kwamba hii ni bahati yao nzuri. Hata hivyo ingeweza pia kusemekana kuwa ya bahati mbaya kwao. Ningependa bado kumkumbusha kila mtu, hata hivyo, kwamba kusudi la Mungu ni sahihi, hata hivyo—tofauti na makusudi ya binadamu, ambayo kila mara ni kuhusu kujifanyia wenyewe mipango na matayarisho. Mnapaswa kuelewa hili, na kutozama katika tafakari zisizoisha. Je, huu sio udhaifu wa binadamu kabisa? Wote wako hivi; badala ya kuwa na upendo mwingi kwa Mungu, wao wana upendo mwingi kwao binafsi. Kwa kuwa Yeye ni Mungu ambaye ni mwenye wivu kwa binadamu, Yeye kila mara huwawekea matakwa. Kadri ambavyo watu hujipenda wenyewe, ndivyo Mungu huwahitaji zaidi wampende Yeye, na ndivyo matakwa Yake kwao huwa makali. Ni kana kwamba Mungu anawachokoza watu kwa kudhamiria. Kama watu wanampenda Yeye kweli, basi inaonekana kuwa Yeye hawatambui. Kwa sababu ya hili, watu wote wanakwaruza vichwa vyao na kubinya masikio yao wanapozama katika tafakari. Hii ni hadithi ya tabia ya Mungu, kutaja kwa ufupi tu kwa jambo moja au mawili. Haya ni mapenzi ya Mungu. Ni kile ambacho Mungu huwataka watu kujua; ni muhimu. Ni kazi mpya, na inalazimu watu kujitahidi ili kupenya na kufanya maendeleo mengine mapya. Je, unaelewa hili? Unataka Niseme mengi zaidi kuhusu mada hii?

Kuhusu enzi za awali, Mungu alisema, “wote walikataliwa na kimya cha barua Yangu. Hii ni kwa sababu watu hao wa kale hawakunitumikia Mimi pekee; kwa hivyo Mimi, kwa malipo Sikuwapenda kipekee. Wao walichukua “zawadi” za Shetani na kisha wakageuka na kunitolea Mimi; Je, hii si kashfa dhidi Yangu?” Maneno haya yanawezaje kuelezwa? Ni kama alivyosema Mungu: “Vipaji vyote hutoka kwa Shetani.” Vizazi vya zamani vya mitume na manabii walitegemea kabisa vipaji vyao walipofanya kazi yao, na kote kote katika enzi, Mungu ametumia vipaji vyao kuendesha kazi Yake. Hii ndiyo maana inasemekana kwamba huduma ya watu wote wenye vipaji hutoka kwa Shetani. Hata hivyo, kama asemavyo Mungu, “Natumia ujanja wa Shetani kama foili^[a]” na hii kwa ajili ya hekima Yake. Hivyo, Mungu amewaita huduma ya watu ambao wana vipaji “zawadi kutoka kwa Shetani” na ni kwa sababu wao ni watu wa Shetani ambao Mungu anaita kitendo hiki “kashfa”. Hii si shutuma isiyo na msingi dhidi ya binadamu; ni ufafanuzi wenye msingi mzuri na wa kufaa. Kwa sababu hii, Alisema, “Sikufichua ghadhabu

Yangu; Mimi nilibadili mpango wao kwa matumizi Yangu mwenyewe kwa kuongezea “zawadi” hizi kwa vifaa Ninavyotumia katika usimamizi Wangu. Baadaye, mara tu vilipokuwa vimesindikwa na mtambo, Ningechema taka zilizo ndani.” Hiki ndicho cha ajabu sana kuhusu kazi ya Mungu. Wazo hili ni la chini mno kukubaliana na fikira za binadamu, kwa sababu hakuna ambaye angefikiri kwamba wale wanaotawala kama wafalme si watu wenye vipaji, ni watu wasio na vipaji ambao Mungu huwapenda. Kama inavyoweza kuonekana, mawazo au matumaini ya Witness Lee na Watchman Nee yote yamegeuka kuwa jivu—na watu wenye vipaji katika siku za sasa sio jambo la pekee. Sasa Mungu ameanza kazi hii, na Anachukua polepole kazi yote ya Roho Mtakatifu ndani ya binadamu ambao huhudumu kama foili kwa kazi Yake. Kazi ya Mungu itakapomalizika kabisa, watu hawa wote watarudi mahali pao pa asili. Hata hivyo, Nawasihi binadamu wasitende kwa kutojali kutokana na kile ambacho Nimesema. Lazima mfuata mkondo, kuzifuata hatua za kazi ya Mungu ili kuepuka kuikatiza. Je, mnaelewa hoja hii? Kwa sababu hii ni hatua na mbinu ya kazi ya Mungu. Wakati ambapo Mungu “atatengeneza” “zawadi” hizi ziwe “bidhaa zilizokamilishwa,” makusudi Yake yote yatakuwa wazi, na zawadi zinazomfanyia Yeye huduma zitaondoshwa zote; hata hivyo, Mungu atakuwa na bidhaa zilizokamilishwa kufurahia. Je, mnaelewa hili? Kile ambacho Mungu hutaka ni bidhaa zilizokamilishwa, sio zawadi za fahari ambazo hutolewa na binadamu. Ni wakati ambapo tu kila mtu amechukua pahali pake pa kufaa, kumaanisha wakati ambapo Mungu amerudi katika nafasi Yake ya asili na shetani, pia, ameketi katika kiti chake, na vilevile malaika, bila kinzano—wakati huo tu ndipo tabasamu ya kupendezwa itaonekana katika uso wa Mungu, kwa sababu makusudi Yake yatakuwa yameridhishwa, lengo Lake limetimizwa. Mungu hatatafuta tena “usaidizi” kutoka kwa “shetani,” kwa sababu makusudi ya Mungu yatakuwa yamefichuliwa kwa dhahiri kwa binadamu, na binadamu kamwe hawatalazimika kuyawasilisha. Wakati huu, miili yao ya tamaa za mwili itakuwa kitu kimoja na roho zao. Hili ndilo Mungu huwafichulia binadamu; ni makusudio ya mwisho ya roho, nafsi, na mwili. Ni muhtasari wa wazo la asili la “ubinadamu.” Hili halihitaji kuchunguzwa kwa utondoti; inatosha kujua jambo moja au mawili kulihusu. Je, mnaelewa?

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Sura ya 36

Inasemekana kwamba Mungu ameanza sasa kuwaadibu watu, lakini hakuna yeyote anayeweza kusema kwa hakika, hakuna yeyote anayeweza kutoa jibu dhahiri iwapo kusudi la asili la kuadibu huku limewafika wanadamu. Mungu asema, “Mwanadamu hajawahi kugundua chochote katika kuadibu Kwangu, kwani hafanyi chochote ila kushika nira inayozunguka shingo

kwa mikono miwili, macho yake mawili yakiwa yamekodolewa Kwangu, kana kwamba anamwangalia adui kwa makini—na wakati huu tu ndio Nahisi vile amedhoofishwa. Ni kwa sababu ya hili ndio Nasema hakuna yeyote aliyewahi kusimama imara katikati ya majaribio.” Mungu humwambia mwanadamu kuhusu ukweli wa kuadibu ambao bado haujamfika, na Yeye hufanya hivyo kwa utondoti mkuu, bila kuacha chochote. Ni kana kwamba wameingia katika kuadibu na hawawezi kweli kusimama imara, Mungu anatoa picha dhahiri yenye kufanana na kiumbe chenye uhai ya uso mbaya wa mwanadamu. Hii ndiyo maana wanahisi kushurutishwa: Kwa vile Mungu asema kwamba mwanadamu hajawahi kamwe kusimama imara katikati ya majaribio, Ningekuware yule anayevunja rekodi ya dunia, kukubaliwa licha ya mila? Wakati huu, wao huanza kutafakari. Kwa kweli, ni kama tu asemavyo Mungu: “Je, Nimewaleta mpaka ukingoni?” Kwa kweli, Mungu amewafikisha watu wote ukingoni, na kwa hiyo, katika fahamu zao, watu daima huamini kwamba Mungu ni mkatili na asiye na huruma. Mungu amewavua watu wote kutoka kwa bahari la mateso ya dunia, baada ya hilo, “ili kuzuia ajali zozote, Niliwaua ‘samaki’ wote waliokuwa wamevuliwa, baada ya hilo samaki hao wakawa watiifu, na hawakuwa na malalamiko hata kidogo.” Je, huu si ukweli? Mungu amewavuta watu wote kutoka kwa bahari ya machungu ya kifo kuingia katika lindi kuu lingine la kifo, amewakokota wote kwa “jiwe kubwa la chakari,” Amewalazimisha kwenda ukingoni—mbona Hafanyi hili kwa wana na watu wengine wa Mungu? Kusudi Lake la kutekeleza kazi kama hii katika nchi ya joka kubwa jekundu ni lipi? Kwa nini mkono wa Mungu ni wenye “nia mbaya” hivyo? Si ajabu “Ninapomhitaji mwanadamu, daima huwa amejificha. Ni kana kwamba hajawahi kamwe kuona maonyesho ya kustaajabisha, kana kwamba alizaliwa mashambani na hajui chochote kuhusu mambo ya mjini.” Kwa kweli, ndani yao watu huuliza: “Mpango wa Mungu katika kufanya hili ni nini? Je, hatuui? Na ya nini? Kwa nini hatua za kazi Yake huja haraka na kwa wingi idadi kubwa, na kwa nini Yeye si mwenye huruma hata kidogo kwetu?” Lakini watu hawathubutu kusema hili, na kwa kuwa maneno ya Mungu huwafanya waache mawazo kama hayo, yakiwanyima nafasi ya kufikiria zaidi, hawana budi ila kuweka kando mawazo yoyote zaidi kama hayo. Ni vile tu Mungu hufichua dhana zote za mwanadamu, na kwa hivyo watu hulazimisha dhana zao kurudi, bila kuziruhusu kujitokeza. Ilisemwa hapo awali kwamba watu hawa ni uzao wa joka kubwa jekundu. Kwa kweli, ili kuwa wazi, wao ni mfano halisi wa joka kubwa jekundu. Mungu anapowalazimisha kufika ukingoni na kuwachinja, basi—bila shaka—roho ya joka kubwa jekundu haina nafasi zaidi ya kufanya kazi ndani yao. Kwa njia hii, watu wanapotembea hadi ukingoni ndio wakati ambapo joka kubwa jekundu hatimaye hufa pia. Inaweza kusemwa kwamba ni kutumia kifo kulipa “wema mkuu wa Mungu”—ambalo ni lengo la kazi ya Mungu katika taifa la joka kubwa jekundu. Watu wanapokuwa tayari kuyatoa maisha yao, kila kitu huwa hafifu, na hakuna anayeweza kuwashinda. Ni nini kingekuwa muhimu zaidi kuliko uzima? Hivyo, Shetani anakuwa hawezi kufanya chochote zaidi ndani ya watu, hakuna

anachoweza kufanya na mwanadamu. Ingawa, katika ufafanuzi wa “mwili” inasemekana kwamba mwili hupotoshwa na Shetani, kama watu watajitoe kweli, na wasiendeshe na Shetani, basi hakuna anayeweza kuwashinda—na wakati huu, mwili utatekeleza kazi yake nyingine, na kuanza kupokea rasmi mwongozo wa Roho wa Mungu. Huu ni mchakato wa lazima, lazima ufanyike hatua kwa hatua; la sivyo, Mungu hangekuwa na njia ya kufanya kazi ndani ya mwili mkaidi. Hiyo ndiyo hekima ya Mungu. Kwa njia hii, watu wote wameingia bila kufahamu katika hali za leo. Na je, si Mungu ambaye amewaongoza watu hadi “mwisho wa barabara”? Je, ingekuwa barabara mpya iliyofunguliwa na mwanadamu? Kwa kutazama uzoefu wenu, inaonekana kwamba ndani yenu, Mungu hutumia mbinu za ukatili mkuu zaidi, ambazo kwazo haki ya Mungu inaweza kuonekana. Mngelosaje kutoa sifa? Kile ambacho Mungu hufanya ndani yenu huwaruhusu watu kutazama tabia ya haki ya Mungu; hili halistahili uvutiwaji wenu kwa Mungu? Leo, katika njia panda wakati ambapo enzi ya zamani bado ipo na enzi mpya bado haijatokea, mnashuhudia vipi kwa Mungu? Suala la maana kama hili halistahili uzingatiaji wa kina? Je, bado mnazingatia mambo mengine, ya nje? Kwa nini Mungu asema “Ingawa wakati fulani watu walitangaza ‘Ufahamu udumu,’ hakuna yeyote ambaye ametumia muda mwingi kuchambua neno ‘ufahamu,’ kuonyesha kwamba watu hawana hamu ya kunipenda”? Kama Mungu hangesema mambo kama hayo, hamngeweza kujaribu kuuelewa moyo wa Mungu kwa hiari yenu wenyewe?

Ingawa, katika nyakati za hivi karibuni, watu wengine huenda wameweza kuja kujua kidogo malengo na wazo la kupata mwili kwa Mungu, Naweza kusema kwa hakika kwamba kama Mungu hangenena kwa wanadamu waziwazi, hakuna yeyote ambaye angeweza kukisia malengo na wazo la kupata mwili kwa Mungu. Hili ni kamili. Je, bado halieleweki kwenu? Kila kitu ambacho Mungu hufanya ndani ya watu ni sehemu ya mpango Wake wa usimamizi—lakini bado hawawezi kuelewa sawasawa mapenzi ya Mungu. Huu ni upungufu wa mwanadamu, lakini Mungu hahitaji kwamba watu wawe na uwezo wa kufanya chochote, Yeye hutaka tu wasikilize “maonyo ya daktari.” Haya ni matakwa ya Mungu. Yeye huwataka watu wote wajue maisha ya mwanadamu ya kweli, kwani “ndani ya mioyo yao, maneno ‘maisha ya mwanadamu’ hayapo, hawayajali, na huchoka tu na maneno Yangu, kana kwamba Nimekuwa bibi mzee mwenye kuparaganya.” Machoni pa watu, maneno ya Mungu ni kama chombo cha siku zote, hawayachukulii kuwa muhimu kabisa. Hivyo, watu hawawezi kuyatia maneno ya Mungu katika vitendo—wamekuwa mafidhuli hafifu wanaofahamu ukweli lakini hawautii katika vitendo. Kosa hili la mwanadamu pekee kwa hivyo linatosha kusababisha chukizo ndani ya Mungu kwa kipindi cha muda, na kwa hiyo Asema mara nyingi kwamba watu hawatilii maanani maneno Yake. Lakini katika dhana zao, watu hufikiria yafuatayo: “Kila siku sisi husoma na kuchambua maneno ya Mungu, ingewezekanaje kusemwa hatuyatilii maanani? Je, huku si kutotutendea kwa haki?”

Lakini wacha Niwachambulie kidogo—watu watakuwa na haya. Wanaposoma maneno ya Mungu, wao huitikia kwa vichwa vyao, wao hunyenyekea mno, kama mbwa wa pua na mdomo mfupi wenye kunyanzi akidorora kwa maneno ya bwana wake. Hivyo, wakati huu, watu huhisi wasiostahili, machozi hutiririka usoni mwao, ni kana kwamba wangependa kutubu na kuanza upya—lakini mara tu wakati huu umepita, kuona aibu kwao hutoweka mara moja, kubadilishwa na hali ya mbwa mwitu, wao huweka maneno ya Mungu upande mmoja, na daima huamini kwamba shughuli zao wenyewe hupewa umuhimu wa kwanza, kwamba mambo ya Mungu huja mwisho, na kwa sababu ya matendo haya yao, huwa hawawezi kamwe kutia maneno ya Mungu katika vitendo. Wakati ukweli unapowasili, wao hunyosha viwiko vyao nje^[a]—huku ni kusaliti watu wao wenyewe—si ajabu Mungu asema, “‘wanakimbia kwenda upande mwingine’ ilhali ananitegemea kwa riziki.” Ni kutoka kwa hili pekee ndio inaweza kuonekana kwamba hakuna uwongo hata kidogo katika maneno ya Mungu, yote ni kweli, na hayana chuku hata kidogo, lakini yanaonekana kuwa yameshindwa kuelezwa kikamilifu kwa kiasi fulani, kwani kimo cha mwanadamu ni kidogo sana, hakina uwezo wa kuyakubali. Maneno ya Mungu tayari yametoa dhihirisho wazi kabisa la mambo ya mwanadamu, ndani na nje, wameyagandisha akilini kwa uwazi kabisa, wakifafanua mfano dhahiri ambao hasa ni sura ya asili ya Shetani. Ni vile tu katika hatua ya sasa, watu bado hawajaona kila kitu kwa dhahiri, na hivyo husemekana kwamba hawajajijua. Ni kwa sababu ya hili ndio Nasema somo hili lazima liendeleo, haliwezi kukoma. Wakati ambapo watu watajijua utakuwa wakati ambapo Mungu atatukuzwa. Hili ni rahisi kuelewa—hakuna haja ya Mimi kuingia katika utondoti. Kunalo, hata hivyo, jambo moja ambalo Nitawakumbusha kuhusu, ingawa kwanza lazima maneno haya ya Mungu yasomwe: “Katika nyakati za leo, watu hawajawahi kunithamini, Sina nafasi ndani ya mioyo yao. Je, wataweza kuonyesha upendo wa kweli Kwangu katika siku zijazo za mateso?” Ni nini maana ya maneno haya? Mungu asema kwamba kuadibu bado hakujamfika mwanadamu, ambalo linaonyesha kwamba bado kuna maana ya ndani ya maneno “kujijua”—je, uliona hili? Bila kupitia taabu na kuadibu, watu wanawezaje kujijua? Haya si maneno matupu? Je, wewe kweli huamini yote yanayonenwa na Mungu? Je, waweza kutambua maneno ya Mungu? Ni kwa nini Mungu husema tena na tena mambo kama “Nionapo matendo ya mwanadamu, chaguo Langu la pekee ni kuondoka,” na pia asema “Ni wakati ambapo tu milima hupinduliwa na dunia kutenganishwa mbalimbali ndio watu hufikiria kuhusu maneno Yangu, wakati huo tu ndio wao huamshwa kutoka kwa ndoto zao, lakini wakati umefika tayari, wamemezwa katika mafuriko makuu, maiti yao yaelea juu ya maji”? Kwa nini Mungu asema, “watu hufikiria juu ya” na sio “watu hutii maneno Yangu”? Ni kweli kwamba milima hupinduliwa na dunia kutenganishwa mbalimbali? Watu hawatilii maanani maneno kama hayo, wao huyaacha yaponyoke, na kwa hiyo wao hupitia “taabu” nyingi katika maneno ya Mungu. Hili ni kwa sababu wao hawajali kabisa. Kwa sababu ya huku kushindwa kwa mwanadamu, Mungu asema “Mimi, ‘dubwasha’ huyu asiye na michirizi

ya machozi, Nimelia machozi mengi kwa ajili ya mwanadamu. Mwanadamu, hata hivyo, hajui lolote kuhusu hili.” Kwa kuwa watu hawatilii maanani maneno ya Mungu, Mungu hutumia njia hii kuwakumbusha na kupata “msaada” wao.

Kwa sasa, Sitatoa unabii kuhusu maendeleo ya ulimwengu, lakini Nitatabiri kitu fulani kuhusu majaliwa ya mwanadamu. Je, Sijataka kwamba watu wajijue? Hili linaweza kuelezwa vipi? Watu wanapaswa kujijua vipi? Mungu “anapowatesa” watu sana kiasi cha wao kukaribia kifo, wao huanza kuelewa jambo fulani kuhusu maana ya maisha ya mwanadamu, na wao huchukia maisha ya mwanadamu, wakiamini kwamba maisha yote ya mwanadamu ni ndoto tu. Wao huamini kwamba maisha ya mwanadamu ni ya uchungu, kwamba watakufa bila kuwahi kutimiza chochote, kwamba maisha yao hayana maana na hayana thamani. Maisha ya mwanadamu ni ndoto tu, ndoto ambayo kwayo huzuni na furaha huja na kuondoka. Leo, watu huishi kwa ajili ya Mungu, lakini kwa kuwa wanaishi katika ulimwengu wa mwanadamu, maisha yao ya kila siku hubaki matupu na bila thamani, kuwafanya watu wote wajue kwamba raha ya Mungu ni faraja ipitayo tu—lakini iwapo, wakati ambapo hawamfurahii Mungu, bado wao huishi ndani ya mwili hata kama wanamwamini Mungu, ya nini? Katika mwili, yote ni matupu kwa mwanadamu. Baada ya kupitia mabadiliko ya maisha ya mwanadamu, kwa majilio ya umri mzee nywele za mwanadamu hupata mvi, uso wake hujaa kunyanzi, mikono yake hufunikwa na sagamba. Ingawa amelipa gharama kubwa, hajapata chochote kwa kweli. Hivyo, maneno Yangu yanaenda hatua moja zaidi: Kila kitu ni kitupu kwa wanaoishi ndani ya mwili. Hili ni bila shaka, na hakuna haja ya wewe kulichunguza hili kwa utondoti. Hii ni sura ya asili ya maisha ya mwanadamu ambayo Mungu amezungumzia mara kwa mara. Mungu hakwepi maneno haya kutokana na udhaifu wa mwanadamu, lakini Hutenda tu kufuatana na mpango Wake wa asili. Labda, maneno mengine hutoa usaidizi na ufahamu kwa watu, na labda mengine hufanya kinyume kabisa, kwa makusudi kusababisha watu kuishi katika mazingira ya kifo—na ni kwa sababu ya hili kabisa ndio wao huteseka. Hivyo, labda Mungu hueleza kinagaubaga “mkakati wa mji mtupu”^[b] ili kuwapotosha watu kimakusudi, lakini hawawezi kuona hili kabisa, wao hubaki gizani. Na bado, yote yako mikononi mwa Mungu, na ingawa watu hulijua hili, wangepoteza kujikinga dhidi ya hilo? Hivyo, hakuna yeyote awezaye kuepuka tishio la kuadibu—wangepoteza nini? Wanaweza tu kutii mipango ya Mungu—na je, hilo si kwa sababu Mungu amewanyakua na hatawaachilia? Ni katika matishio ya Mungu tu ndiyo watu wote wanaweza kufuata hali ya asili ya maisha—je, hii si kweli? Kama sio mipango ya Mungu, watu wangepoteza kukubali kushindwa kwa hiari? Huo haungekuwa mzaha? Ingawa maisha ya mwanadamu ni matupu, nani yuko radhi, wakati ambapo maisha yake yana starehe, kuachana kimyakimya na ulimwengu wa mwanadamu na kujaribu kumridhisha Mungu? Watu hufa katikati ya kutojiweza—nani amewahi kufa katikati ya utele, wakati ambapo ana yote ambayo angeweza kutaka? Ni “nyota” iliyoshuka kutoka angani

tu ingekuwa isiyofuata kawaida kwa jambo hili. Ikilinganishwa na maisha ya mbingu ya tatu iliyo furahia, maisha duniani yangukuwa sawa na kuishi jahanamu—ni katika hali kama hiyo tu ndiyo ingeweza kuwa radhi kufa. Lakini nani leo hii ni nyota mbinguni? Mimi, pia, “Sielewi” kuhusu hili. Hebu tutafute kila mahali tuone kama tunaweza kupata mmoja. Iwapo atapatikana, Naomba watu wanisaidie kuuliza iwapo yuko radhi kutenda kufuatana na maneno Yangu yaliyo hapo juu. Lakini Nina onyo kwa kila mmoja wenu: Hakuna kati yenu anatakiwa kujisingizia “shujaa” na kujitolea kufa, mnaelewa?

Tanbihi:

a. “Nyoo sha kiwiko cha mtu nje” ni nahau ya Kichina, ambayo inamaanisha mtu anawasaidia wengine kwa gharama ya watu walio karibu na mtu huyo, kwa mfano wazazi, watoto, jamaa au ndugu.

b. “Mkakati wa jiji tupu” ni sehemu ya 32 ya Mikakati ya Thelathini na Sita ya China ya kale. Mkakati huu unajumuisha kuwasilisha taswira ya kujiamini ili kuficha ukosefu wa kuwa tayari ili kumhadaa adui.

Sura ya 38

Kufuatana na sifa za asili za wanadamu, yaani, uso halisi wa wanadamu, kuweza kuendelea hadi sasa hakujakuwa jambo rahisi kweli, na ni kwa njia hii tu ndio nguvu kuu ya Mungu imekuwa dhahiri. Kutegemea kiini cha mwili pamoja na upotovu wa joka kuu jekundu hadi sasa, isingekuwa uongozi wa Roho wa Mungu, mwanadamu angeweza kusimama leo? Mwanadamu hastahili kuja mbele ya Mungu, lakini Anawapenda wanadamu kwa ajili ya usimamizi Wake na ili kazi Yake kuu iweze kufanikishwa kabla ya muda mrefu sana. Kwa kweli, hakuna mtu anayeweza kulipa upendo wa Mungu kwa wanadamu katika maisha yao yote. Labda wengine wanataka kulipa neema ya Mungu kwa kuyatoa maisha yao, lakini Nakwambia: Mwanadamu hastahili kufa mbele ya Mungu, na kwa hiyo kifo cha mwanadamu ni bure. Kwa sababu kwa Mungu kifo cha mwanadamu hakistahili hata kutajwa, wala hakina thamani ya senti moja, na ni kama kifo cha chungu duniani. Ninashauri binadamu wasiwe wa kuweka thamani kubwa sana juu yao wenyewe, na msifikirie kuwa kufa kwa ajili ya Mungu kunabeba uzito wa mlima mkubwa. Kwa Kweli, kifo cha mwanadamu ni suala jepesi kama unyoya. Hakistahili kutambuliwa. Lakini tena, mwili wa mwanadamu umeandikiwa kufa kwa asili, na hivyo mwishoni, maumbile ya mwili yanapaswa kuishia duniani. Huu ni ukweli mwaminifu, na hakuna anayeweza kuukanusha. Hii ni “sheria ya asili” ambayo ninaitoa kutokana na ujumla wa maisha ya binadamu, na kwa hivyo, Mungu amefafanua mwisho wa mwanadamu kwa njia hii wote wa maisha ya binadamu, bila yeyote kujua. Je, unaelewa? Si ajabu Mungu anasema “Ninadharau uasi wa wanadamu. Sijui kwa nini; inaonekana ni kana kwamba Nimemchukia mwanadamu tangu mwanzo, na bado Ninahisi huruma kubwa kwake. Hivyo ndivyo watu daima wamekuwa na mitazamo miwili kunihusu—kwa kuwa Nampenda mwanadamu, na pia Namchukia.”

Nani asiyemtukuza Mungu kwa kuwepo Kwake au kuonekana Kwake? Kwa wakati huu, ni kama kwamba Nimesahau kabisa uchafu na udhalimu ndani ya mwanadamu. Kujidai kwa wanadamu, kujikweza, kutotii, kutojali, na uasi wake wote—Nayasukuma haya yote nyuma ya mawazo Yangu ili kuyasahau. Mungu hazuiliwi kwa sababu ya nafsi kama hiyo ya wanadamu. Kwa kuwa Mungu na Mimi “tunashiriki mateso haya haya,” nami pia Nitajiondoa kwenye shida hii ili Nisizuiliwe zaidi na mwanadamu. Kwa nini ujisumbue na hilo? Kwa kuwa mwanadamu hayuko radhi kujiunga na nyumba ya Mungu pamoja nami, Nitawezaje kutumia nguvu Zangu kuwakomesha? Sifanyi mambo kulazimisha nguvu Zangu kwao, na si ajabu, kwa sababu Nilizaliwa katika jamii ya Mungu, bila shaka mwanadamu na Mimi daima ni tofauti. Hili limesababisha kushindwa mno kwa leo. Lakini Naendelea kuepukana na udhaifu wa mwanadamu; Nina chaguo gani? Je, si hili ni kwa sababu Mimi sina uwezo? Si ajabu Mungu anataka “kustaafu” kutoka katika “wakala” wa wanadamu, na anataka “pensheni” Yake. Nanena kutokana na mtazamo wa mwanadamu, na mwanadamu hasikilizi, lakini Ninenapo kama Mungu, je, bado haasi? Labda siku itakuja ambapo Mungu kwa kweli “atastaafu” ghafla kutoka katika “wakala” wa wanadamu, na wakati huo utakapokuja, neno la Mungu litakuwa kali zaidi. Leo, inaweza kuwa kwa sababu Yangu ndio Mungu ananena hivi, na siku hiyo ikija, Mungu hatakuwa tena kama Mimi, kwa subira “akiwatambia watoto hadithi katika shule ya chekechea.” Labda kile Nisemacho si cha kutanianakabisa lakini Mungu ana nia ya kulegeza mshiko pekee kwa sababu ya Mungu aishiye, la sivyo, ingekuwa ya kutisha sana kutafakari. Kama vile Mungu alisema, “Nililegeza fumbato Langu kwao kwa kiasi fulani, kuwaruhusu kujiingiza katika tamaa zao za mwili, na hivyo walithubutu kuwa jeuri, bila kizuizi, na inaweza kuonekana kuwa hawanipendi kweli, kwa vile wote wanaishi katika mwili.” Kwa nini Mungu anasema hapa “kujiingiza katika tamaa zao,” na “kuishi katika mwili” hapa? Ukweli usemwe, mwanadamu kwa kawaida ataelewa maneno kama haya bila ufafanuzi Wangu. Labda watu wengine wanasema hawaelewi, lakini Nitakwambia kuwa unajua ukweli, na unajifanya tu hujui. Nakukumbusha: Kwa nini Mungu anasema “Mimi Namwomba mwanadamu kushirikiana Nami tu”? Kwa nini Mungu anasema kuwa asili ya binadamu ni ngumu kubadilika? Kwa nini Mungu hudharau asili ya binadamu? Na asili ya mwanadamu ni nini hasa? Asili ya mwanadamu si nini? Nani amezingatia maswali haya? Pengine hii ni mada mpya kwa mwanadamu, lakini haijalishi, Namwomba mwanadamu aifikirie sana, la sivyo utamchukiza Mungu daima kwa sababu ya maneno kama “asili ya binadamu haiwezi kubadilika.” Kuna maana gani katika kutenda kinyume Chake kwa njia hiyo? Je, huko si kutafuta shida? Je, mwishowe, si kama tu kurusha yai dhidi ya jiwe?

Kwa kweli, majaribio na majaribu yote yanayomjia mwanadamu ni masomo ambayo Mungu anahitaji kwa mwanadamu. Kufuatana na nia ya asili ya Mungu, mwanadamu anaweza

kutimiza vitu hivi hata kama mwanadamu atastahili kutoa kama dhabihu kile anachopenda, lakini, kwa sababu mwanadamu daima anajipenda tu, kwa hiyo anashindwa kushirikiana kweli na Mungu. Mungu hataki mengi kutoka kwa mwanadamu. Yote ambayo Mungu anataka kwa mwanadamu yanahitaji kutimizwa kwa urahisi na kwa furaha; ni vile tu mwanadamu hayuko radhi kupitia shida. Kama watoto, angeweza kuishi kwa uangalifu ili kupata senti chache kuwaheshimu wazazi wake na kutimiza wajibu anaopaswa kutimiza. Lakini anaogopa kwamba hatakula vizuri vya kutosha na kwamba mavazi yake yatakuwa ya kawaida sana, kwa hiyo kwa sababu moja au nyingine, anachukua upendo na utunzaji wa wazazi wake na kuvitupa mbali sana katika mawingu, kama kwamba atanza kufanya hili baada ya kupata kiasi kikubwa cha fedha. Lakini Naweza kuona kutokana na hili kwamba wanadamu hawana utiifu wa mapenzi wa kuwapenda wazazi wao—ni wana wasio na mapenzi kwa wazazi. Pengine hili ni kali mno, lakini Siwezi kufoka upuuzi kinyume na ukweli. Siwezi “kuwaiga wengine” ili kumpinga Mungu kwa kujiridhisha Mwenyewe. Ni kwa sababu hakuna mtu hapa duniani aliye na upendo wa watoto kwa wazazi ndio Mungu alisema: “Mbinguni, Shetani ni adui Yangu, duniani, mwanadamu ni adui Yangu. Kwa sababu ya muungano kati ya mbingu na dunia, vizazi tisa vyao vinapaswa kuchukuliwa kuwa na hatia kwa ushirikiano.” Shetani ni adui wa Mungu; sababu Ninayosema hiyo ni kwa sababu hamlipi Mungu kwa neema na fadhili Zake, lakini badala yake “hupiga kasia kinyume na mkondo,” na kwa kufanya hivyo hatimizi “utiifu wa kuwapenda wazazi” kwa Mungu. Je, watu hawako hivi pia? Hawaonyeshi heshima ya upendo kwa “wazazi” wao na hawalipi malezi na msaada wa “wazazi” wao. Hili linatosha kuonyesha kwamba watu wa dunia ni jamaa ya Shetani mbinguni. Mwanadamu na Shetani ni wa moyo mmoja na akili moja dhidi ya Mungu, na kwa hiyo si ajabu Mungu anahusisha vizazi tisa kama wenye hatia kwa ushirikiano na hakuna anayeweza kusamehewa. Katika siku za nyuma, Mungu alikuwa na mtumishi mnyenyekevu kusimamia wanadamu, lakini hakusikia, na akafanya kulingana na silika yake ya kuasi dhidi Yake. Je, si wanadamu waasi pia wanapiga hatua mbele kwenye njia hii? Haijalishi ni kiasi gani Mungu anakaza “hatamu,” watu hawatikisiki kamwe tu na hawawezi kugeuka. Kwa maoni yangu, kama mwanadamu ataendelea kwa njia hii, ataharibiwa, na labda ni wakati huu ndio utaelewa maana halisi ya maneno haya: “mwanadamu hawezi kujifundua kwa asili yake ya kale?” Mungu amemkumbusha mwanadamu mara nyingi: “Kwa sababu ya uasi wa mwanadamu, Nimemwacha.” Kwa nini Mungu anasema hivi tena na tena? Je, Mungu anaweza kuwa katili hivyo? Kwa nini Mungu anasema pia “Mimi si mwanadamu hasa”? Kwa siku nyingi zilizotulia, ni nani ambaye amechunguza kweli masuala haya kwa kina? Nawahimiza wanadamu waweke juhudi zaidi katika maneno ya Mungu na wasiyachukulie kwa wepesi; hili halina faida kwako, au kwa wengine. Ni vyema kutosema kile ambacho hakihitajiki kusemwa, na kutofikiri juu ya kile ambacho hakihitajiki kuzingatiwa. Je, hilo si rahisi zaidi? Je, ni kosa gani linaweza kutokana na hili? Kabla ya Mungu kutangaza mwisho wa kazi Yake duniani, hakuna mtu ataacha “kusonga”;

hakuna mtu atakayejitoe kabisa katika wajibu wake. Sasa sio wakati; usijifanye kuwa kiongozi kwa Mungu, au mtangulizi. Nadhani ni mapema sana kukoma sasa na kuacha kusonga mbele—unaonaje?

Mungu humleta mwanadamu katika kuadibu, na Huwaingiza katika mazingira ya kifo, lakini kwa upande mwingine, ni nini ambacho Mungu anataka mwanadamu afanye duniani? Kujifanya kama kabati la nguo nyumbani? Haliwezi kuliwa au kuvaliwa, bali kutazamwa tu. Ikiwa ni hivyo, kwa nini utumie michakato mingi migumu, kuwafanya watu wateseke sana katika mwili? Mungu Asema, “Namsindikiza kwenye ‘uwanja wa kuua,’ kwa kuwa hatia ya wanadamu inatosha kustahili kuadibu Kwangu.” Kwa wakati huu, je, Mungu anawafanya watu watembee kwenda kwa uwanja ya kuua wenyewe? Kwa nini hakuna mtu anayewaomba msamaha? Basi, mwanadamu anapaswa kushirikiana jinsi gani? Je, mwanadamu anaweza kufanya mambo kweli bila kuathiriwa na hisia, kama Mungu Anavyofanya hukumu Zake? Ufanisi wa maneno haya hasa unategemea matendo ya mwanadamu. Kama baba anavyopata pesa, ikiwa baadaye mama hajui jinsi ya kushirikiana, bila kujua jinsi ya kusimamia nyumba, basi nyumba hiyo itakuwa katika hali gani? Angalia hali ya kanisa sasa; Je, nyinyi kama viongozi mtafikiria nini? Nyinyi mnaweza kuwa na mkutano ambapo kila mtu anaweza kuzungumza kuhusu fikira zao kibinafsi. Mama hufanya machafuko ya vitu nyumbani, kwa hiyo watoto wa familia hii watakuwa kama nani? Mayatima? Waombaji? Si ajabu Mungu alisema: “Watu wote wanadhani kwamba Mimi ni uungu unaokosa ‘ubora wa akili,’ lakini ni nani anayeweza kuelewa kwamba Naweza kubaini kila kitu katika ubinadamu?” Kuhusu hali dhahiri kama hiyo, hakuna haja ya kuzungumza kutoka kwa uungu Wake. Kama alivyosema Mungu, “hakuna haja ya kugonga msumari kwa nyundo kubwa.” Kwa wakati huu, labda kuna watu wengine ambao wana uzoefu wa vitendo na neno la Mungu la hekima: “Miongoni mwa wanadamu, hakuna yeyote anayenipenda.” Wakati huu, ni vile tu alivyosema Mungu: “Watu wote wanainamisha vichwa vyao kwa kusita kwa sababu ya hali ya sasa, lakini mioyo yao bado haijaridhika.” Maneno haya ni kama darubini. Katika siku za karibu za usoni, mwanadamu ataingia katika hali nyingine. Hii inaitwa kutorekebisha. Je, mnaelewa? Hilo ndilo jibu kwa maswali haya mawili ya Mungu: “Je, watu hawaepuki dhambi tu kwa sababu wanaogopa Nitaondoka? Je, si kweli kwamba hawalalamiki tu kwa sababu wanaogopa kuadibu?” Kwa kweli, sasa watu ni wazembe kidogo na wanaonekana wamechoka sana, na hawajali kabisa kutilia maanani kazi ya Mungu, na wanajishughulisha tu na utaratibu na mipango ya miili yao. Je, huu si ukweli?

Sura ya 39

Hebu twende nje ya maneno ya Mungu na tuzungumze kidogo juu ya masuala yanayohusu

maisha yetu, ili maisha yetu yasitawi, na tufikie matumaini ya Mungu kwetu. Hasa, pamoja na ujaji wa leo—wakati wa kila mmoja kuainishwa kulingana na aina, na wa kuadibu—kuna haja kubwa ya kuyalenga mambo muhimu na kumakinikia “maslahi ya pamoja.” Haya ni mapenzi ya Mungu, na kile kinachopaswa kutimizwa na watu wote. Tungewezaje kukosa kujitolea kwa ajili ya mapenzi ya Mungu mbinguni? Mungu “hutoa idadi kwa kila aina ya watu na Huweka alama tofauti kwa kila aina ya mtu, ili babu zao waweze kuwaongoza kurudi kwa jamii zao,” ambalo linaonyesha kuwa watu wameainishwa kulingana na aina, na kutokana na hilo, kila aina za watu wanafichua umbo lao halisi. Kwa hivyo, ni haki kusema kuwa watu ni waaminifu kwa babu zao, sio kwa Mungu. Hata hivyo, watu wote pia wanatoa huduma kwa Mungu kwa uongozi wa babu zao, ambao ni ajabu ya kazi ya Mungu. Vitu vyote vinamhudumia Mungu, na hata kama Shetani anawasumbua watu, Mungu hutumia fursa hii kutumia “rasilimali za mahali hapo” kumhudumia. Watu, hata hivyo, hawawezi kutambua hili. Kama Mungu Anavyosema, “hivyo, Nagawa kazi pia, na kusambaza juhudi. Hii ni sehemu ya mpango Wangu, na hauwezi kuvurugwa na mtu yeyote.” Watu hawawezi kuona yote yanayodhamiriwa na Mungu, na yote ambayo Mungu anataka kufanikisha, kabla ya Yeye kuyafanya. Wanaweza kuyaona tu wakati ambapo kazi ya Mungu imekamiliwa; kama sivyo, wao ni vipofu, na hawaoni chochote.

Leo, Mungu ana kazi mpya miongoni mwa makanisa. Yeye Hufanya kila kitu kifuate hali ya asili ya maisha, kwa kweli kutumia kazi ya mwanadamu. Kama Mungu anavyosema, “Natawala kila kitu miongoni mwa vitu vyote, Naamuru kila kitu miongoni mwa vitu vyote, Nikisababisha vyote vilivyoko kufuata hali halisi ya maisha na kutii amri ya asili.” Sijui ni utambuzi mahiri gani mlilo nao katika “kufuata hali ya asili ya maisha,” basi hebu tuzungumze kuhusu hili. Hivi ndivyo Ninavyoliona: Kwa sababu wanaongozwa kwenda nyumbani na babu zao, watu wa aina zote wanapaswa kutokea na “kutekeleza.” Na kwa sababu wanafuata hali ya asili ya maisha, kile ambacho ni cha asili kwao kinatumika kutumia kazi yao ya asili, kikiwafanya kufuata mwongozo wa Roho Mtakatifu kulingana na mwelekeo huu wa kawaida. Kazi ya Roho Mtakatifu hutekelezwa kulingana na hali iliyo ndani ya kila mtu; kusema kweli, hii inaitwa “Mungu hushawishi vitu vyote ili vimhudumie,” hili basi linahusiana na kufuata hali ya asili ya maisha. Ingawa mtu ana vitu vya asili ya shetani ndani yake, Mungu atavitumia hivi, Akiongeza kazi ya Roho Mtakatifu kwa msingi wa kile kilicho ndani yake kwa asili, Akiwafanya kutosha kutoa huduma kwa Mungu. Haya ndiyo yote Nitakayosema kuhusu “kufuata hali ya asili ya maisha”—labda mna mapendekezo mengine makuu zaidi. Natumaini mnaweza kutoa maelezo fulani ya thamani, au vipi? Je, mko tayari kushirikiana katika kufuata hali ya asili ya maisha? Je, mko tayari kugawanya kazi na Mungu? Mmewahi kufikiria kuhusu jinsi ya kuitimiza hili? Natumaini kwamba watu wanaweza kuelewa mapenzi ya Mungu, kuwa wanaweza kuwa wenye mawazo sawa katika kumridhisha Mungu kwa ajili ya maadili ya

pamoja, na wanaweza kuendelea pamoja katika njia ya kuelekea kwa ufalme. Kuna haja gani ya kuja na dhana zisizohitajika? Ni kuweco kwa nani kufikia leo hakujakuwa kwa ajili ya Mungu? Na kwa kuwa ni hivyo, kuna haja gani ya huzuni, ghamu, na tanafusi? Hili halina faida kwa mtu yeyote. Maisha yote ya watu yapo mikononi mwa Mungu, na isingekuwa kwa ajili ya azimio lao mbele ya Mungu, ni nani angekuwa radhi kuishi bure katika dunia hii tupu ya mwanadamu? Kwa nini ujisumbue? Kurupuka ndani na nje ya ulimwengu, wasipomfanyia Mungu chochote, je, maisha yao yote hayatakuwa ya bure? Hata kama Mungu hayaoni kwamba matendo yako yanastahili kutajwa, je, hutatoa tabasamu la kuridhika wakati wa kifo chako? Unapaswa kufuatilia maendeleo ya kujenga, sio kurudi nyuma hasi—je, huu sio utendaji bora? Kama matendo yako ni kwa ajili ya kumridhisha Mungu kabisa, basi hutakuwa hasi au wa kurudi nyuma. Kwa sababu daima huwa kuna mambo ambayo hayaeleweki mioyoni mwa watu, bila wao kutambua nyuso zao zimefunikwa na mawingu ya giza, ambalo husababisha kuonekana kwa “mitaro” kadhaa katika nyuso zao bila wao kujua, ambayo inaonekana ni kwa sababu ardhi inaendelea kupasuka. Ni kama kwamba ardhi inaendelea kusonga, ikisababisha “viduta” au “miteremko” juu ya ardhi kusongeza mahali bila watu kutambua. Katika hili, Siwadhihaki watu, bali Nazungumzia “maarifa ya kijiografia.”

Ingawa Mungu amewaongoza watu wote katika kuadibu, Hasemi chochote juu ya hili. Badala yake, Anaepuka mada hii kwa makusudi na kuanza mpya, ambalo katika suala moja ni kwa sababu ya kazi ya Mungu, na katika lingine, ni ili kukamilisha mara moja hatua hii ya kazi. Kwa sababu malengo ya Mungu katika kutekeleza hatua hii ya kazi yalitimizwa kitambo, hakuna haja ya kusema chochote zaidi. Leo, sijui ni kiasi gani mmeona kuhusu mbinu za kazi ya Mungu; katika ufahamu Wangu, siku zote Mimi Huhisi kuwa kazi ya Mungu haijagawanywa kwa dhahiri katika hatua na vipindi vya muda kama ilivyokuwa awali. Badala yake, kila siku huleta njia zake za kufanya kazi, mabadiliko hutokea karibu kila siku tatu hadi tano, na hata katika siku tano, kunaweza kuwa na aina mbili tofauti za maudhui kwa kazi ya Mungu. Hili linaonyesha kasi ya kazi ya Mungu; kabla ya watu kuwa na muda wa kufurahia na kuangalia kwa makini, Mungu ashaenda asionekane tena. Hivyo, Mungu daima Hashikiki kwa watu, ambalo limesababisha kutotambulika kwa kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa nini Mungu daima Husema maneno kama “na kwa hiyo Nilimwacha mwanadamu”? Watu wanaweza kuzingatia kidogo maneno haya, lakini hawaelewi maana yake. Na je, wakati huu, mnaelewa? Si ajabu watu hawana ufahamu wa kuwepo kwa Roho Mtakatifu. Kutafuta kwao kwa Mungu daima huwa chini ya mwanga wa mwezi usio dhahiri—hili ni kweli kabisa—na ni kama kwamba Mungu anamtania mwanadamu kwa makusudi, Akifanya mabongo ya watu wote kufura, ili wahisi kizunguzungu na kukanganyika. Wao hujua wanachofanya kwa taabu sana, ni kama kwamba wanaota, na mara wanapoamka, hawajui kilichotokea. Kinachohitajika tu ni maneno machache ya kawaida kutoka

kwa Mungu kuwafanya watu wasijue la kufanya. Si ajabu, basi, kwamba Mungu asema, “Leo, Nawatupa watu wote katika ‘tanuru kubwa’ ili wasafishwe. Nasimama juu kuangalia kwa makini watu wakichomeka motoni na, kwa kulazimishwa na miale ya moto, watu wanatoa ukweli.” Katikati ya maneno ya Mungu yanayobadilika daima, watu hawajui la kufanya; kwa kweli, kama tu Mungu anavyosema, kuadibu kumeanza kitambo, na kwa sababu watu hawajatambua jambo hili, wanajua tu wakati Mungu anaposema hivyo wazi wazi, wao huwa makini tu baada ya Mungu kuwaambia. Inaweza kusemwa kuwa watu huanza tu kuchunguza kuhusu kuadibu sasa kwa vile kazi ya Mungu imetekelezwa kufikia kiwango hiki. Ni kama tu wakati ambapo watu walitambua bomu la atomiki—lakini kwa sababu wakati haujafika, watu hawatilii maanani; wakati mtu anapoanza tu kulitengeneza ndio watu huanza kuwa makini. Ni wakati ambapo bomu la atomiki linapoonekana tu ndio watu huelewa zaidi kulihusu. Mungu anaposema tu Atamtupa mwanadamu ndani ya tanuru ndio watu hufahamu kidogo. Kama Mungu hangezungumza, hakuna ambaye angejua—je, si sivyo? Kwa hiyo, Mungu asema, “watu wanaingia ndani ya tanuru bila kujua, kama kwamba wameongozwa huko kwa kamba, kama kwamba hawasikii.” Kwa nini usichanganue hili: Wakati watu wanapotoa ukweli, je ni wakati ambapo Mungu anasema kwamba kuadibu kumeanza, au kabla ya wakati ambapo Mungu anasema kwamba kuadibu kumeanza? Kutokana na hili inaweza kuonekana kuwa, kabla ya Mungu kunena juu ya kuadibu, watu walianza kukiri, kuonyesha kwamba kuadibu kulianza kabla ya Mungu kuzungumza juu yake—je, huu si ukweli?

Sura ya 40

Kwa Mungu, mwanadamu ni kama mtu anayechezewa katika mshiko Wake, kama nudo inyoshwayo kwa mkono katika mikono Yake—inayoweza kufanywa nyembamba au nzito kama apendavyo Mungu, kuifanyia Apendavyo. Ni haki kusema kwamba mwanadamu kwa kweli ni mtu anayechezewa mikononi mwa Mungu, kama paka wa Uajemi ambaye bibi amemnunua kutoka sokoni. Bila shaka, yeye ni mtu anayechezewa mikononi mwa Mungu—na kwa hiyo hakukuwa na chochote cha uongo kuhusu ufahamu wa Petro. Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba maneno na matendo ya Mungu ndani ya mwanadamu hutimizwa kwa wepesi na raha, bila kuhangaika. Yeye hapigi bongo Lake au kufanya mipango, kama wanavyofikiri watu; kazi ambayo Yeye hufanya ndani ya mwanadamu ni ya kawaida sana, kama yalivyo maneno ambayo Yeye hutamka kwa mwanadamu. Mungu anapozungumza, Yeye huonekana kusema jambo ambalo hakukusudia kusema, Yeye husema chochote kinachoringia akilini Mwake, bila kizuizi. Hata hivyo, baada ya kusoma maneno ya Mungu, watu huridhishwa kabisa, wao hukosa maneno, wakikodoa macho na kuduwaa. Ni nini kinaendelea hapa? Hili huonyesha vizuri hasa jinsi hekima ya Mungu ilivyo kuu. Kama, jinsi wanavyofikiri watu, kazi ya Mungu ndani ya mwanadamu ilibidi ipangwe kwa uangalifu sana ili iwe barabara na sahihi,

basi—ili kupeleka fikiria hizi hatua moja mbele zaidi—hekima ya Mungu, ajabu, na kutoeleweka vingeweza kupimwa kiasi chake, inayoonyesha ukadiriaji wa watu kuhusu Mungu ni duni sana. Kwa sababu daima huwa kuna ujinga ndani ya matendo ya watu, wao humtathmini Mungu kwa njia hiyo hiyo. Mungu hafanyi mipango au mipangilio kuhusu kazi Yake; badala yake, hiyo hutekelezwa moja kwa moja na Roho wa Mungu—na kanuni ambazo kwazo Roho wa Mungu hufanya kazi ni huru na bila simile. Ni kana kwamba Mungu hatilii maanani hali za mwanadamu na huzungumza Apendavyo—lakini bado mwanadamu hujiondoa kwa maneno ya Mungu kwa shida, ambayo ni kwa sababu ya hekima ya Mungu. Ukweli, hata hivyo, ni ukweli. Kwa sababu kazi ya Roho wa Mungu ndani ya watu wote ni dhahiri sana, hii inatosha kuonyesha kanuni za kazi ya Mungu. Kama Mungu angehitajika kulipa gharama kubwa hivyo katika kazi Yake ndani ya viumbe vilivyoubwa, hiyo haingekuwa hali ya kutumia mbao nzuri kwa matumizi duni? Je, ni lazima Mungu atende binafsi? Je, ingekuwa na thamani? Kwa kuwa Roho wa Mungu amekuwa akifanya kazi kwa muda mrefu sana, lakini kotekote katika enzi Roho wa Mungu hajawahi kufanya kazi kwa njia hii, hakuna ambaye amewahi kujua njia na kanuni ambazo kwazo Mungu hufanya kazi, hazijawahi kuwa wazi. Leo ziko wazi, kwani Roho wa Mungu amezifichua binafsi—na hii ni bila shaka, inaonyeshwa moja kwa moja na Roho wa Mungu, sio kufupishwa na mwanadamu. Mbona usifunge safari kwenda kwa mbingu ya tatu na uone kama hili ndilo linaloendelea kwa kweli, uone kama, baada ya kufanya kazi hii yote, kazi za Mungu zimemwacha mchovu, mgongo Wake ukimuuma na miguu Yake ikiwa na maumivu, au hata kutoweza kula au kulala; na iwapo ilikuwa ni lazima Asome vifaa vingi sana vya marejeleo ili kuzungumza maneno haya yote, iwapo miswada ya matamshi ya Mungu yametandazwa kote mezani, na iwapo Amekauka mdomoni kutokana na kusema maneno mengi. Ukweli ni kinyume kabisa: Maneno ya hapo juu hayako sawa na mahali ambapo Mungu huishi. Mungu asema, “Nimetumia wakati mwingi, na kulipa gharama kubwa, kwa ajili ya mwanadamu—lakini wakati huu, kwa sababu isiyojulikana, dhamiri za watu zimesalia zisizoweza kamwe kutekeleza shughuli zao za asili.” Haijalishi kama watu wana ufahamu wowote wa huzuni ya Mungu, kama wanguweza kukaribia upendo wa Mungu bila kwenda kinyume cha dhamiri yao, hili lingechukuliwa kuwa la kirazini na la maana. Hofu ya pekee ni kwamba hawako radhi kutumia kazi ya asili ya dhamiri. Je, wasemaje, hii ni sahihi? Je, maneno haya yanakusaidia? Tumaini Langu ni kwamba mtakuwa wa aina ya vitu vilivyo na dhamiri, badala ya kuwa takataka isiyo na dhamiri. Mnafikiri nini kuhusu maneno hayo? Je, kuna yeyote anayefahamu hili? Kudungwa sindano ndani ya mioyo yenu hakuwaumizi? Mungu hudunga sindano ndani ya maiti isiyohisi? Je, Mungu amekosea, uzee umefifisha uwezo Wake wa kuona? Nasema hilo haliwezekani! Hata hivyo, hili lazima liwe ni kosa la mwanadamu. Mbona msiende hospitalini na mtazame? Bila shaka kuna tatiza na moyo wa mwanadamu, unahitaji kuwekewa “viungo” vipya—mwaonaje kuhusu hilo? Mngefanya hilo?

Mungu asema, “Mimi huziangalia sura zao mbaya na vioja, na Mimi huondoka kwa mwanadamu tena. Chini ya hali kama hizi, watu husalia wasiofahamu, na huchukua tena vitu Nilivyowanyima, wakingoja kurudi Kwangu.” Mbona, wakati wa “enzi hii mpya ya teknolojia,” Mungu bado anazungumza juu ya mkokoteni unaovutwa na ng’ombe? Ni kwa nini? Je, ni kwa sababu Mungu hupenda kusumbua? Je, Mungu anapitisha tu muda kwa sababu Hana jingine bora la kufanya? Je, Mungu ni kama mwanadamu, kupoteza tu wakati baada ya kujishindilia chakula? Kuna maana yoyote ya kurudia maneno haya tena na tena? Nimesema kwamba watu ni mafidhuli, kwamba lazima kila mara uwanyakue kwa masikio ili uwasiliane nao. Baada ya maneno kunenwa kwao leo, watayasahau mara moja kesho—ni kana kwamba wanasumbuliwa na usahaulifu. Hivyo, sio ukweli kwamba maneno mengine hayajananenwa, bali ni kwamba hayajatimizwa na watu. Kama jambo fulani linasemwa mara moja au mara mbili tu, watu wanasalia kuwa wajinga—lazima lisemwe mara tatu, hii ndiyo namba ya chini zaidi. Hata kuna “wazee” wengine ambao lazima lisemwe mara kumi hadi ishirini kwao. Kwa njia hii, jambo hilo hilo husemwa tena na tena katika njia tofauti, kuona kama watu wamebadilika au la. Je, mmefanya kazi kweli kwa njia hii? Sitaki kuwagombeza watu, lakini wote wanamfanyia Mungu dhihaka; wote wanajua kuchukua vijalizo vya rutubishi, lakini hawahisi hamu kwa ajili ya Mungu—na je, huku ni kumhudumia Mungu? Huku ni kumpenda Mungu? Si ajabu wao hushinda siku nzima bila kujali kitu chochote, kuhusu wavivu na watulivu. Lakini hata hivyo, watu wengine bado hawajaridhika, na wao husababisha huzuni yao wenyewe. Labda Ninakuwa mkali kidogo, lakini hili ndilo linajulikana kama kuwa mwepesi wa kuvutwa na kujipenda! Je, ni Mungu ambaye hukufanya uhisi mwenye huzuni? Je, hii si hali ya kuleta mateso juu yako mwenyewe? Je, neema yoyote ya Mungu haina sifa inayostahili kuwa chanzo cha furaha yako? Kotekote, hujakuwa mzingatifu wa mapenzi ya Mungu, na umekuwa mhasi, mdhaifu, na mwenye dhiki—mbona ni hivyo? Je, ni mapenzi ya Mungu kukufanya uishi katika mwili? Hamjui mapenzi ya Mungu, msio na utulivu ndani ya mioyo yenu wenyewe, ninyi hunung’unika na kulalamika, na kushinda siku nzima mkikunja uso, na miili yenu hupata maumivu na mateso—hilo ndilo mnalostahili! Mnawaambia wengine wamsifu Mungu kati ya kuadibu, kwamba waibuke kutoka kwa kuadibu, na wasizuiwe nako—lakini ninyi mmeingia ndani yake na hamuwezi kuhepa. Inachukua miaka mingi kuiga hii “roho ya kujitoa mhanga” kama ya Dong Cunrui. Unapohubiri maneno na kanuni, huoni aibu? Je, wajijua mwenyewe? Umejiweka kando? Unampenda Mungu kweli? Umeweka kando matazamio na majaliwa yako? Si ajabu Mungu husema kwamba watu ndio walio wa ajabu na wasioeleweka. Nani angefikiri kwamba kuna “hazina” nyingi sana ndani ya mwanadamu ambazo hazijachimbwa? Leo, mandhari yake yanatosha “kufungua macho ya mtu”—watu ni “wa ajabu” sana! Ni kana kwamba Mimi ni mtoto asiyeweza kuhesabu. Hata leo bado Sijaelewa ni watu wangapi wanampenda Mungu kweli. Siwezi kamwe kukumbuka idadi—na kwa hiyo, kwa sababu ya “kuasi” Kwangu, wakati

unapofika wa kutoa hesabu mbele ya Mungu, Mimi kila mara huwa mikono mitupu, Nisiyeweza kufanya vile Ningependa, Mimi kila mara huwa katika deni la Mungu. Kutokana na hilo, Nitoapo hesabu, Mimi kila mara “hukemewa” na Mungu. Sijui ni kwa nini watu ni katili sana, kila mara wao hunifanya Niteseke kwa ajili ya hili. Watu hutumia nafasi hii kuangua kicheko, wao si marafiki Wangu kweli. Nikiwa katika matatizo, wao hawanipi msaada wowote, lakini hunifanyia mzaha kwa makusudi—wao kweli hawana dhamiri!

Sura ya 41

Mungu humfanyanga mwanadamu vipi? Je, unalifahamu hili? Linaeleweka? Nalo hufanyika vipi kanisani? Unafikiriaje? Je, umewahi kuyafikiria maswali haya? Ni nini ambalo Anatarajia kufanikisha kupitia kwa kazi Yake kanisani? Je, yote yanaeleweka bado? Kama sivyo, yote ambayo unafanya hayana maana, yamebatilika! Je, maneno haya yanaugusa moyo wako? Je, yote ambayo yanahitajika kutimiza tamanio la Mungu ni maendeleo ya utendaji tu, na sio kuwa hasi na kurudi nyuma? Je, ushirikiano wa kijinga unatosha? Je, unapaswa kufanya nini kama bado kuna wingu la utata kuhusu maono? Je, ni sawa kutotafuta? Mungu asema, “Wakati mmoja Nilianza shughuli kubwa miongoni mwa wanadamu, lakini hawakutambua, kwa hivyo ilibidi Nitumie neno Langu ili kuwafichulia. Na hata hivyo, bado mwanadamu hangeweza kuyaelewa maneno Yangu, na akasalia kutojua malengo ya mpango Wangu.” Hili linamaanisha nini? Je, umewahi kufikiria kusudi lake? Je, Mungu hutenda tu bila sababu na kijinga? Na ikiwa ni hivyo, ya nini? Iwapo kusudi si dhahiri, na iwapo mwanadamu haelewi, basi anawezaje kushirikiana kwa kweli? Mungu asema kwamba ukimbizaji wa watu uko ndani ya bahari zisizo na mipaka, ndani ya maneno matupu na mafundisho ya dini. Ninyi hamwezi hata kusema ukimbizaji wenu upo katika kundi lipi. Ni nini ambacho Mungu anataka kutimiza ndani ya mwanadamu? Unapaswa kuelewa mambo haya yote. Je, ni kwa ajili tu ya kuliaibisha joka kubwa jekundu katika hali hasi? Yawezekana kwamba baada ya kuliaibisha joka kubwa jekundu, Mungu ataishi tu kama mtawa asiye na chochote? Basi ni nini ambacho Mungu anataka? Je, kweli Anaitaka mioyo ya wanadamu? Au maisha yao? Au utajiri na mali yao? Hivi vina maana gani? Havina maana kwa Mungu. Je, Mungu amefanya mengi sana ndani ya mwanadamu ili Aweze tu kuwatumia kama ushahidi wa ushindi Wake juu ya Shetani, na kudhihirisha nguvu Zake? Hili halingemfanya Mungu aonekane mwenye kujishughulisha na mambo finyu? Je, kweli Mungu ni Mungu wa aina hiyo? Kama tu mtoto anayewasababisha watu wazima kugombana? Hili lina umuhimu gani? Mwanadamu daima amemchunguza Mungu kupitia kwa fikira zake mwenyewe. Mungu alisema wakati mmoja, “Mwaka una majira manne, na kwa kila majira kuna miezi mitatu.” Mwanadamu alisikiliza, na akayakumbuka maneno Yake, na akaendelea kusema kwamba kulikuwa na miezi mitatu kwa kila majira na majira manne kwa mwaka. Na kisha, Mungu alipouliza, “Kuna majira mangapi katika mwaka? Na miezi mingapi kwa kila majira?”

wanadamu wakajibu kwa maafikiano, “Majira manne, miezi mitatu.” Mwanadamu daima hujaribu kumfafanua Mungu kwa kutegemea sheria fulani. Siku hizi katika enzi ya “majira matatu kwa kila mwaka, miezi minne kwa kila majira,” mwanadamu bado hafahamu, inavyoonekana ni mjinga, inaonekana amekuwa kipofu huku akitafuta sheria katika kila kitu. Na sasa mwanadamu anajaribu kutumia amri zake kwa Mungu! Yeye ni mjinga kweli! Haoni sasa hakuna “majira ya baridi,” bali “majira ya kuchipua, majira ya joto, na majira ya majani kupukutika” pekee? Mwanadamu kweli ni mpumbavu! Katika hali ya sasa, mwanadamu bado hafahamu namna ya kumjua Mungu. Yeye ni kama tu watu wa miaka ya 1920, wanaofikiria kwamba njia za usafirishaji ni sumbufu, kwa hivyo wanatembea, au wanatumia punda, au wanaofikiria wanapaswa kutumia taa za mafuta, au njia zingine za kale za maisha. Je, hizi zote si fikira kutoka kwa akili za wanadamu? Kwa hiyo ya nini hata hivyo kuzungumza juu ya huruma na upendo leo? Hili lina maana gani? Kama bikizee anayeparaganya, akisimulia siku zake zilizopita, haya maneno yana maana gani? Hata hivyo, wakati wa sasa ni wakati wa sasa; je, saa inaweza kurudishwa nyuma kwa miaka 20 au 30? Watu kila mara hufuata mkondo; kwa nini ni vigumu sana wao kulielewa hilo. Katika enzi hii ya sasa ya kuadibu, mazungumzo haya ya huruma na upendo yana maana gani? Kana kwamba yote yanayomhusu Mungu ni huruma na upendo? Ni kwa nini katika enzi hii ya “unga na mchele,” watu wanaendelea kulisha watu makapi ya mtama na mboga za porini? Lile ambalo Mungu hataki kulifanya, kwa lazima, mwanadamu anamkomesha kwa nguvu. Kama Angepinga, Angepachikwa jina la “mpinga mapinduzi,” na ingawa ilisemwa tena na tena kwamba Mungu hakuwa mwenye huruma au mwenye upendo, nani angesikiliza? Mwanadamu ni mpuuzi sana. Inaonekana neno la Mungu halina athari. Kila mara wanadamu huyafikiria maneno Yangu kwa njia tofauti. Kila mara Mungu hudhulumiwa na watu, na inaonekana kwamba watu wasio na hatia wanakabiliwa na shtaka lisilo na msingi; ni nani atatenda kulingana na Mungu? Kila mara ninyi mko tayari kuishi katika huruma na upendo wa Mungu, kwa hiyo ni kipi ambacho Mungu astahili kufanya kando na kustahimili matusi ya mwanadamu? Hata hivyo, Natumai mnaweza kufahamu jinsi Roho Mtakatifu hufanya kazi kabla ya kubishana na Mungu. Hata hivyo, Nawasihi sana mfahamu maana ya asili ya neno la Mungu. Usifikiri kwamba wewe ni mwerevu, na kufikiri kwamba neno la Mungu lina najisi. Hili si lazima! Ni nani anaweza kusema ni kiasi gani cha “najisi” kiko ndani ya neno la Mungu? Isipokuwa Mungu aliseme moja kwa moja, au kulionyesha kwa dhahiri. Usijivune sana. Kama mnaweza kuona njia ya kufanya mazoezi kutokana na maneno Yake, basi ninyi mmetimiza masharti. Mnataka kuona nini kingine? Mungu alisema “Sina huruma yoyote tena kwa udhaifu wa mwanadamu.” Hata maneno haya dhahiri, na rahisi hayawezi kufafanuliwa, kwa hiyo mbona uhangaika bure kufanya utafiti, na kufanya uchunguzi zaidi? Bila hata maarifa ya msingi ya uhandisi, mwanadamu angewezaje kustahili kuunda roketi? Je, huyo si mtu tu anayependa kujisifu? Mwanadamu hastahili kuifanya kazi ya Mungu; ni kwa

sababu tu Mungu humkuza. Bila kujua Anachopenda, Anachochukia, na kumhudumia tu. Je, hii si mbinu ya kusababisha msiba? Wanadamu hawajielewi, lakini wanafikiri wao ni wa ajabu. Wanafikiri wao ni nani! Wao ni wajinga kweli kuhusu tofauti kati ya mema na maovu. Kumbuka wakati uliopita, na utazame mbele kwa siku za baadaye. Je, unafikiri nini? Kisha upate kujijua.

Mungu amefichua mengi sana kuhusu nia na kusudi la mwanadamu. Mungu alisema, “Ulikuwa wakati huu ambapo Niliona nia na kusudi la mwanadamu. Nilishusha pumzi kutokana na kushindwa kuelewa: Ni kwa nini siku zote lazima mwanadamu atende kwa ajili ya maslahi yake? Je, kuadibu Kwangu hakukusudii kumkamilisha? Je, Najaribu kumvunja moyo?” Ni nini ambacho unajifunza kujihusu kutokana na maneno haya? Je, nia na kusudi la mwanadamu vimeenda kwa kweli? Umewahi kupeleleza? Ni heri muweze kuja mbele za Mungu ili mjifunze, kazi Yake ya kuadibu hutimiza nini ndani yenu? Je, mmefanya muhtasari wake? Labda kiasi kidogo sana, la sivyo huenda mngejiingiza katika kutia chumvi kitambo. Ni nini ambacho Mungu anawataka mtimize? Kuhusu maneno ambayo mmezungumziwa, ni kiasi gani ambacho mmetia katika vitendo? Ni kiasi gani kilisemwa bure? Machoni pa Mungu, kiasi kidogo cha maneno Yake hutekelezwa kwa kweli; hii ni kwa sababu mwanadamu hawezi kamwe kutambua maana Yake ya asili, naye hukubali tu maneno yoyote yanayorudiwa. Kwa njia hii anaweza kuyajua mawazo ya Mungu? Hivi karibuni, Mungu atakuwa na kazi nyingi kwa ajili ya mwanadamu; je, mwanadamu anaweza kuifanikisha kazi hiyo kwa kimo kidogo alichu nacho mwanadamu sasa? Kama si mwenye kosa, mwanadamu ni mpumbavu, au labda mwenye kiburi, asili za watu ni kama hizi. Halieleweki kwa kweli: Kutokana na yote ambayo Mungu amesema, kwa nini mwanadamu haathiriwi nayo? Yawezekana kwamba neno la Mungu ni mzaha tu, lisilonuiwa kuwa na athari yoyote? Yote kwa ajili ya kumwona mwanadamu akiigiza mchezo wa “Furaha, Hasira, Huzuni, na Shangwe”? Ili kumfanya mwanadamu afurahi kwa wakati mmoja, na alie kwa wakati mwingine, na baadaye akitenda kama aonavyo kuwa bora nje ya jukwaa? Hili lingekuwa na athari gani? “Kwa nini matakwa Yangu kwa mwanadamu kila mara huambulia patupu? Je, ni kana kwamba Nilikuwa Namtaka mbwa apande mti? Je, Najaribu kuleta taabu bila sababu?” Maneno yote ya Mungu hulenga hali halisi ya mwanadamu. Haitakuwa na manufaa yeyote kutazama ndani ya watu wote ili aone ni nani anaishi kulingana na neno la Mungu. “Na bado sasa, sehemu kubwa ya mandhari inaendelea kubadilika. Kama siku moja dunia itabadilika kwa kweli kuwa aina nyingine, Nitaiweka kando bila kusita—je, hiyo si hatua ambayo Niko ndani sasa katika kazi Yangu?” Kwa kweli, Mungu yuko katika mchakato wa kazi hii sasa; hata hivyo, Mungu anapotaja “kuweka kando bila kusita,” hii inahusu siku za baadaye, kwa kuwa kila kitu ni mchakato. Je, unaweza kuona kwamba huu ndio mwelekeo katika kazi ya Mungu ya sasa? Kwa ajili ya dosari ya nia ya mwanadamu, pepo wachafu huchukua nafasi ya kujidhihirisha. Wakati huu, “dunia itabadilika kuwa aina nyingine” na watu wakati huo

watabadilika kwa ustahilifu, lakini kiini chao kitabaki vilevile. Hii ni kwa sababu kuna kitu kingine katika dunia ya kuendeleza. Kwa maneno mengine, dunia ya asili ilikuwa duni, na mara tu ikishaendelezwa inaweza kutumika. Hata hivyo, baada ya dunia kutumiwa kwa kipindi fulani, na kisha isitumiwe tena, itarudi polepole kwa umbo lake la asili. Huu ni muhtasari wa hatua inayofuata ya kazi ya Mungu. Kazi ya Mungu ya siku za baadaye itakuwa ngumu zaidi kufahamika, kwa sababu ni wakati wa kuainisha aina mbalimbali za watu. Katika mahali pa mkutano pa mwisho, patakuwa machafuko ya fujo, na mwanadamu hatakuwa na maoni yenye msimamo. Kama tu alivyosema Mungu: “Wanadamu wote ni wachezaji wanaokubaliana na kundi.” Jinsi wanadamu walivyo na uwezo wa kucheza ili kukubaliana na kundi, Mungu hutumia dosari hii kwa ajili ya hatua inayofuata katika kazi Yake, ili aweze kuwafanya wanadamu wote wageuze kasoro hii. Ni kwa sababu hawana kimo halisi kuwa wanadamu ni kama panzi juu ya ukuta. Wangukuwa nacho, wangukuwa miti yenye uwezo mkuu. Mungu anakusudia kutumia sehemu ya kazi ya pepo wachafu ili kuikamilisha sehemu ya mwanadamu, ili watu hawa waweze kufahamu matendo ya mapepo, na kuwawezesha watu wote wawafahamu kwa kweli mababu zao. Ni kwa njia hii pekee wanadamu wanaweza kujinasua kabisa, sio tu kutoroka kizazi cha mapepo, lakini hata zaidi mababu wao. Hili ndilo kusudi la asili la Mungu kulishinda kabisa joka kubwa jekundu, kufanya hivyo ili wanadamu wote wajue umbo halisi la joka kubwa jekundu, Aambue kinyago chake kabisa, na kuona umbo lake halisi. Hili ndilo Mungu anataka kutimiza, nalo ni lengo Lake la mwisho duniani ambalo Amefanyia kazi nyingi sana; Ananua kulifanikisha hili ndani ya watu wote. Hili linajulikana kama ushawishi wa vitu vyote kwa ajili ya kusudi la Mungu.

Je, mnaelewa jinsi kazi ya siku za usoni itafanywa? Haya yote lazima yaeleweke. Kwa mfano: Kwa nini Mungu asema kwamba wanadamu kamwe hawashughulikii wajibu wao? Kwa nini Anasema kwamba watu wengi wamekosa kukamilisha zoezi ambalo Amewaachia? Vitu hivi vinaweza kutimizwa vipi? Je, umewahi kuyafikiria maswali haya? Haya yamekuwa mada ya mawasiliano yako? Kwa ajili ya hatua hii ya kazi, mwanadamu lazima aelewe makusudi ya Mungu ya sasa. Mara tu hilo likishatimizwa, mengine yanaweza kujadiliwa, ni sawa? Kile ambacho Mungu anatarajia kutimiza ndani ya mwanadamu kinahitaji kuelezwa kabisa, la sivyo haina faida. Hawataweza kuingia ndani yake, na hata huenda isiwezekane kwa wao kulitimiza; ni ya kinadharia tu. Je, mmepata njia ya kufanya mazoezi ya kile ambacho Mungu amesema hivi sasa? Watu hulizingatia neno la Mungu kwa hisia ya woga. Hawawezi kulifahamu, na wanaogopa kumkosea Mungu. Wamepata njia ngapi za kula na kunywa ambazo zimetajwa sasa? Wengi hawajui namna ya kula na kunywa; hili linaweza kutatuliwa vipi? Je, mlipata njia ya kufanya hivyo katika tamko la leo? Ulijaribu kushirikiana kwa njia gani? Na nyote mkishayasikia maneno, huwa mnajadiliana fikira zenu kwa njia gani? Je, mwanadamu hapaswi

kufanya hili? Ni jinsi gani unapaswa kuagiza matumizi ya dawa sahihi? Bado unahitaji sauti ya wazi ya Mungu? Je, hili linahitajika? Matatizo haya yanawezaje kukomeshwa kabisa? Hii inategemea iwapo unaweza kushirikiana na Roho Mtakatifu katika matendo na ushirikiano ufaao. Kama kuna ushirikiano wa kufaa, Roho Mtakatifu atafanya kazi kuu. Ikiwa hakuna ushirikiano wa kufaa bali kwa usahihi zaidi ni rabsha, Roho Mtakatifu hatakuwa na uwezo wa kusaidia. “Kama unamjua adui yako na kujijua, utaibuka mshindi kila mara.” Bila kujali yule aliyenena maneno haya kwanza, ni ya kukufaa wewe zaidi. Kwa ufupi, lazima kwanza mjijue kabla ya kuweza kuwajua maadui zenu, na hatimaye mtaweza kushinda kila vita. Lazima nyote muweze kufanya hili. Haijalishi kile ambacho Mungu anataka kutoka kwako, unahitaji tu kujitolea kikamilifu. Natarajia utaweza kuonyesha uaminifu wako kwa Mungu mbele Yake mwishowe, na maadamu unaweza kuiona tabasamu ya Mungu ya kupendeza Akiwa katika kiti Chake cha enzi, hata kama ni wakati wako kufa, lazima uweze kucheka na kutabasamu macho yako yanapofumba. Lazima umfanyie Mungu wajibu wako wa mwisho wakati wa muda wako hapa duniani. Zamani, Petro alisulubiwa juu chini kwa ajili ya Mungu; hata hivyo, unapaswa kumridhisha Mungu mwishowe, na utumie nguvu zako zote kwa ajili ya Mungu. Kiumbe anaweza kumfanyia Mungu nini? Kwa hiyo unapaswa kujitolea kwa rehema ya Mungu mapema iwezekanavyo. Maadamu Mungu anafurahia na Anapendezwa, basi mwache Afanye chochote Atakacho. Wanadamu wana haki gani ya kulalamika?

Sura ya 42

Sijui kama watu wameona mabadiliko yoyote katika tamko la leo. Huenda watu wengine wameona kidogo, lakini hawathubutu kusema kwa kweli. Labda wengine hawajatambua chochote. Mbona kuna tofauti kubwa sana hivyo kati ya siku ya kumi na mbili na ya kumi na tano ya mwezi? Umetafakari hili? Maoni yako ni gani? Umeelewa chochote kutokana na matamko yote ya Mungu? Ni kazi gani kuu iliyofanywa kati ya tarehe mbili Aprili na tarehe kumi na tano Mei? Mbona, leo, watu wanaonekana hawana habari, wamekanganywa kama kwamba walikuwa wamegongwa na rungu kichwani? Leo, mbona hakuna safu zinazoitwa “Kashfa za Watu wa Ufalme”? Tarehe mbili na tarehe nne za Aprili, Mungu hakuonyesha hali ya mwanadamu; vilevile, katika siku kadhaa baada ya leo Hakuonyesha hali ya watu—mbona hivyo? Kwa hakika kuna fumbo kuhusu hili—kwa nini kulikuwa na mgeuko kabisa? Hebu kwanza tuzungumze kidogo kuhusu kwa nini Mungu alinena hivyo. Hebu tuyaangalie maneno ya Mungu ya kwanza, ambayo kwayo Hakupoteza wakati kusema “Punde tu kazi mpya inapoanza.” Sentensi hiyo inakupa fununu ya kwanza kwamba kazi ya Mungu imeingia katika mwanzo mpya, kwamba Ameanza kazi mpya kwa mara nyingine. Hili linaonyesha kwamba kuadibu kunakaribia kumalizika; inaweza kusemwa kwamba kilele cha kuadibu tayari kimeingiwa, na kwa hiyo lazima mtumie wakati wenu vyema ili mpitie vizuri kazi ya enzi ya

kuadibu, ili msibaki nyuma na msiachwe. Hii yote ni kazi ya mwanadamu, na inahitaji kwamba mwanadamu afanye kila awezalo kushirikiana. Wakati ambapo kuadibu kumeondolewa kabisa, Mungu anaanza kuanzisha sehemu inayofuata ya kazi Yake, kwani Mungu asema, "... Nimeendelea kutekeleza kazi Yangu miongoni mwa wanadamu.... Wakati huu, moyo Wangu umejaa furaha kuu, kwani Nimepata sehemu ya watu, na kwa hiyo 'biashara' Yangu haiko tena katika hali ya kuporomoka, si maneno matupu tena." Katika nyakati zilizopita, watu waliona mapenzi ya Mungu ya dharura katika maneno Yake—hakuna uwongo ndani ya hili—na leo Mungu anafanya kazi Yake kwa kasi kuu zaidi. Kwa mwanadamu, hili halionekani kulingana kabisa na matakwa ya Mungu—lakini kwa Mungu, kazi Yake tayari imemalizika. Kwa kuwa mawazo ya watu ni magumu sana kueleweka, fikira yao kuhusu mambo mara nyingi huwa yenye utata mno. Kwa kuwa watu wanadai mengi kutoka kwa watu, lakini Mungu hamdai mwanadamu mengi sana, inaonyesha jinsi tofauti kati ya Mungu na mwanadamu ilivyo kuu. Dhana za watu huwekwa wazi katika yote ambayo Mungu hufanya. Sio kwamba Mungu huwadai watu makuu na watu hawawezi kuyafikia, lakini kwamba watu humdai Mungu makuu na Mungu hawezi kuyatimiza. Kwa sababu, baada ya matibabu, kuna athari ya ugonjwa wa awali ndani ya mwanadamu, ambaye amepotoshwa na Shetani kwa miaka elfu kadhaa, watu daima wamemtaka Mungu atende mambo "makuu" kama hayo, na hawana huruma hata kidogo, wakiogopa sana kwamba Mungu hapendezwi. Hivyo, kwamba watu hawawezi kufanya kazi katika mambo mengi ni njia ambayo wanajisababishia adhabu; wanapitia athari za matendo yao wenyewe, na hayo ni mateso matupu. Kuhusu taabu inayovumiliwa na watu, zaidi ya asilimia 99 inadharauliwa na Mungu. Kusema waziwazi, hakuna mtu ambaye ameteseka kweli kwa ajili ya Mungu. Wote huvumilia athari za matendo yao wenyewe—na hii hatua ya kuadibu, bila shaka, si tofauti, ni mwiba wa kujidunga, ambao anachukua na kujidunga. Kwa kuwa Mungu hajafichua kusudi halisi la kuadibu Kwake, ingawa kuna sehemu ya watu ambao wamelaaniwa, hili haliwakilishi kuadibu. Sehemu ya watu wamebarikiwa, lakini hili halina maana kwamba watabarikiwa katika siku za baadaye. Kwa watu, inaonekana kwamba Mungu ni Mungu asiyetimiza neno Lake. Usijali. Huenda haya yakawa yamepita mipaka, lakini usiwe hasi; Ninachozungumzia kina uhusiano fulani na kuteseka kwa mwanadamu, lakini Nafikiri lazima uunde uhusiano mwema na Mungu. Lazima umpe "zawadi" nyingi zaidi, hilo bila shaka litamfurahisha. Naamini kwamba Mungu huwapenda wanaompa "zawadi." Unasema nini, maneno haya ni sahihi?

Kufikia sasa, mmeacha kiasi gani cha matarajio yenu? Kazi ya Mungu itamalizika hivi punde—kwa hiyo lazima muwe mmeacha takribani matarajio yenu yote, sivyo? Mnaweza hata hivyo kujichunguza: Mnapenda kila mara kujiamini, mkijiinua na kujitangaza—hii ni nini? Leo, bado Sijui matarajio ya watu ni gani? Kama watu kweli wanaishi wakiwa wamezingirwa na bahari ya mateso, wanapoishi katikati ya utakaso wa taabu, au chini ya tishio la vifaa mbalimbali

vya mateso, au wanapoishi wakati wa kukataliwa na watu wote na kutazama angani na kutanafusi kwa uzito, katika mawazo yao nyakati kama hizi wanaweza, labda, kuyaacha matarajio yao. Hii ni kwa sababu watu hutafuta paradiso ya kufikirika katikati ya kutokuwa na matumaini, na hakuna mtu ambaye katika hali za starehe amewahi kuacha ufukuziaji wake wa ndoto nzuri. Hii huenda ikawa ndoto, lakini Ningependa kwamba hili silo jambo lililo ndani ya mioyo ya watu. Je, bado mnataka kunyakuliwa mkiwa hai? Je, bado mnataka kubadilisha umbo lenu katika mwili? Sijui kama mna maoni sawa, lakini kila mara Nimehisi kwamba hii ni ndoto—mawazo kama haya huonekana ya kupita kiasi sana. Watu husema mambo kama haya: Acha matarajio yako, kuwa wa kweli. Unataka watu waachane na mawazo ya kubarikiwa—lakini wewe je? Wewe hukanushi mawazo ya watu ya kubarikiwa na wewe mwenyewe unatafuta baraka? Huwaruhusu wengine kupokea baraka lakini wewe unazifikiria kwa siri—hilo linakufanya kuwa nini? Tapeli? Unapofanya hivyo, dhamiri yako haishutumiwi? Ndani ya moyo wako, huhisi kuwa na deni? Je, wewe si mdanganyifu? Unachimbua maneno yaliyo ndani ya mioyo ya wengine, lakini husemi lolote kuhusu yaliyo moyoni mwako—wewe kweli ni kipande cha takataka kisicho na thamani! Nashangaa mnachofikiria ndani ya mioyo yenu mnapozungumza—hamngeweza kushutumiwa na Roho Mtakatifu? Hili halifadhaishi hadhi yenu? Kweli hamjui kinachowafaa! Inadhihirika kwamba nyinyi nyote ni kama Bw. Nanguo—nyinyi ni walaghai. Si ajabu Mungu aliweka “kujitolea” ndani ya “wote wako radhi ‘kujitolea’” katika mabano. Mungu anamfahamu sana mwanadamu, na haijalishi jinsi udanganyifu wa mwanadamu ulivyo wa kijanja—hata asipofichua chochote, uso wake haubadiliki rangi kuwa mwekundu, moyo wake hauendi kasi—macho ya Mungu yanang'aa, kwa hiyo mwanadamu kila mara amekuwa na tatizo kuepuka kuangaza macho kwa Mungu. Ni kana kwamba Mungu ana mwanga wa eksirei na anaweza kuziona sehemu zilizo ndani ya mwili wa mwanadamu, kana kwamba Anaweza kufahamu watu wana aina gani ya damu bila upimaji. Hekima ya Mungu ni kama hiyo, na haiwezi kuigwa na mwanadamu. Kama asemavyo Mungu, “Kwa nini Nimefanya kazi nyingi sana, lakini hakuna thibitisho lake ndani ya watu? Je, kwani Sijatia bidii ya kutosha?” Ushirikiano wa mwanadamu na Mungu una upungufu mno, na inaweza kusemwa kwamba kuna mengi sana yaliyo hasi ndani ya mwanadamu, na watu huwa na matumaini yoyote kwa shida sana, wao huwa nayo kiasi kidogo mara chache tu, lakini yametiwa doa sana. Hili linaonyesha tu watu wanampenda Mungu kiasi gani; ni kana kwamba kuna sehemu mia kwa milioni ya kumpenda Mungu ndani ya mioyo yao, kati ya hiyo asilimia 50 bado imetiwa doa, ndiyo maana Mungu anasema hapati thibitisho lolote ndani ya mwanadamu. Ni kwa sababu ya kutotii kwa mwanadamu hasa ndio sauti ya matamko ya Mungu ni katili sana na isiyo na huruma. Ingawa Mungu haneni na mwanadamu kuhusu nyakati ambazo zimepita, watu kila mara hutaka kukumbuka ya kale, ili kujionyesha mbele ya Mungu, na wao kila mara hutaka kuzungumza juu ya nyakati ambazo zimepita—lakini Mungu hajawahi kuchukulia jana ya

mwanadamu kama leo; badala yake, Yeye huwashughulikia watu wa leo kwa kutumia leo. Huu ni mtazamo wa Mungu, na katika hili, Mungu ameyasema maneno haya kwa dhahiri, ili kuwazuia watu kusema katika siku zijazo kwamba Mungu hafikirii mno, kwani Mungu hafanyi mambo ya kupita kiasi, bali huwaambia watu ukweli, watu wasije wakakosa kuweza kusimama imara—kwani mwanadamu, hata hivyo, ni mnyonge. Baada ya kuyasikia maneno haya, unasemaje kuyahusu: Je, uko radhi kusikia na kutii, na kutoyafikiria zaidi?

Yaliyo hapo juu yako nje ya mada, haijalishi kama yanazungumziwa au la. Natumai hamtakuwa tofauti, kwa sababu Mungu anakuja kufanya kazi hii ya maneno, na Hupenda kuzungumza kuhusu kila kitu chini ya jua. Lakini Natumai bado mtayasoma, na hamtapuuza maneno haya, Sawa? Mngefanya hivyo? Ilisemwa tu kwamba katika maneno ya leo Mungu amefichua habari mpya: Mbinu ambayo kwayo Mungu hufanya kazi iko karibu kubadilika. Kwa hivyo, ingekuwa bora kulenga mada hii motomoto. Inaweza kusemwa kwamba matamko yote ya leo yanatabiri masuala ya siku za baadaye, yanahusu Mungu kufanya mpango kwa ajili ya hatua inayofuata ya kazi Yake. Mungu karibu amemaliza kazi Yake ndani ya watu wa kanisa, baadaye Atatumia ghadhabu kuonekana mbele ya watu wote. Kama asemavyo Mungu, “Nitawafanya watu walio duniani wakubali mambo Yangu, na mbele ya ‘kiti cha hukumu,’ matendo Yangu yatathibitishwa, ili yakubalike miongoni mwa watu walio kote duniani, ambao watasalimu amri.” Je, uliona chochote ndani ya maneno haya? Humu mna muhtasari wa sehemu inayofuata ya kazi ya Mungu. Kwanza, Mungu atawafanya walinzi wote wanaotawala kwa nguvu za kisiasa waridhike kabisa na wajiondoe katika jukwaa la historia, kutowahi kupigania hadhi tena au kufanya hila na kula njama. Kazi hii lazima itekelezwe kwa njia ya Mungu kusababisha mabaa mbalimbali duniani. Lakini Mungu hataonekana; kwa sababu, wakati huu, nchi ya joka kubwa jekundu bado itakuwa ni nchi ya uchafu, Mungu hataonekana, lakini ataibuka tu kwa njia ya kuadibu. Hiyo ndiyo tabia ya Mungu yenye haki, na hakuna anayeweza kuiepuka. Katika wakati huu, vyote vinavyoishi katika taifa la joka kubwa jekundu vitapitia maafa, ambavyo kwa kawaida ni pamoja na ufalme ulio duniani (kanisa). Huu ndio hasa wakati ambao ukweli hujitokeza, na kwa hiyo unapitiwa na watu wote, na hakuna anayeweza kuepuka. Hili limejaaliwa na Mungu. Ni kwa sababu ya hatua hii ya kazi hasa ndio Mungu asema, “Huu ndio wakati wa kutekeleza mipango mikuu.” Kwa sababu, katika siku za baadaye, hakutakuwa na kanisa duniani, na kwa ajili ya majilio ya machafuko, watu wataweza tu kufikiria kuhusu kile kilicho mbele yao na watapuuza kila kitu kingine, na ni vigumu kwao kumfurahia Mungu katikati ya machafuko, hivyo, watu wanatakiwa kumpenda Mungu kwa moyo wao wote katika wakati huu wa ajabu, ili wasikose nafasi. Ukweli huu unapopita, Mungu amelishinda kabisa joka kubwa jekundu, na hivyo kazi ya ushuhuda wa watu wa Mungu imefika mwisho; baadaye Mungu ataanza hatua inayofuata ya kazi, Akifanya uharibifu kwa nchi ya joka kubwa jekundu,

na hatimaye kuwagongomelea watu juu chini msalabani kotekote katika ulimwengu, baadaye Atawaangamiza wanadamu wote—hizi ni hatua za siku za baadaye za kazi ya Mungu. Hivyo, mnapaswa kutaka kufanya lote muwezalo kumpenda Mungu katika mazingira haya ya amani. Katika siku za baadaye hamtakuwa na nafasi zaidi za kumpenda Mungu, kwani watu huwa tu na nafasi ya kumpenda Mungu katika mwili; wanapoishi katika ulimwengu mwingine, hakuna atakayenena kuhusu kumpenda Mungu. Je, hili si jukumu la kiumbe aliyeumbwa? Kwa hiyo unapaswa kumpenda Mungu vipi katika siku zako za uhai? Umeshawahi kufikiri juu ya hili? Je, unangoja mpaka ufe ili umpende Mungu? Je, haya si maneno matupu? Leo, kwa nini hufuatilii kumpenda Mungu? Je, kumpenda Mungu huku ukiwa na shughuli nyingi kunaweza kuwa upendo halisi wa Mungu? Madhumuni ya kusema kwamba hatua hii ya kazi ya Mungu itafika mwisho hivi punde ni kwa sababu Mungu tayari ana ushuhuda mbele ya Shetani; hivyo, hakuna haja ya mwanadamu kufanya lolote, mwanadamu anatakiwa tu kufuatilia kumpenda Mungu katika miaka ambayo yuko hai—hili ndilo jambo muhimu. Kwa sababu masharti ya Mungu si mengi, na, zaidi ya hayo, kwa kuwa kuna hamu kuu ndani ya moyo Wake, Amefichua muhtasari wa hatua inayofuata ya kazi kabla ya hatua hii ya kazi kumalizika, ambalo linaonyesha kwa dhahiri kuna kiasi gani cha muda: kama Mungu hangekuwa na hamu ndani ya moyo Wake, je, Angeyanena maneno haya mapema hivyo? Ni kwa sababu muda ni mfupi ndio maana Mungu anafanya kazi kwa njia hii. Inatarajiwa kwamba mnaweza kumpenda Mungu kwa mioyo yenu yote, kwa akili zenu zote, na kwa nguvu zenu zote, jinsi tu mnavyotunza maisha yenu wenyewe. Je, haya siyo maisha yenye maana kuu zaidi? Ni wapi pengine ambapo mngeweza kupata maana ya maisha? Je, ninyi si vipofu kabisa? Uko radhi kumpenda Mungu? Je, Mungu anastahili upendo wa mwanadamu? Je, watu wanastahili ibada ya mwanadamu? Kwa hiyo, unapaswa kufanya nini? Mpende Mungu kwa ujasiri, bila kusita, na uone kila ambacho Mungu atakufanya. Uone kama Atakuchinja. Kwa muhtasari, kazi ya kumpenda Mungu ni muhimu zaidi kuliko kunukuu na kuandika mambo kwa ajili ya Mungu. Unapaswa kukipa kipaumbele kilicho muhimu zaidi, ili maisha yako yaweze kuwa ya thamani zaidi na yajae furaha, na kisha unapaswa kusubiri “hukumu” ya Mungu kwako. Nashangaa iwapo mpango wako utahusisha kumpenda—Ningependa kwamba mipango ya watu wote iwe ile inayokamilishwa na Mungu, na iwe ya uhalisi.

Sura ya 44 na 45

Tangu wakati ambapo Mungu alipomwambia mwanadamu kuhusu “upendo kwa Mungu”—somo la maana zaidi kati ya yote—Alilenga kuzungumza juu ya mada hii katika “matamko ya Roho saba,” kusababisha watu wote kujaribu kujua utupu wa maisha ya mwanadamu, na hivyo kuchimbua upendo wa kweli ulio ndani yao. Na wale wanaoishi katika hatua ya sasa wanampenda Mungu kiasi gani? Je, mwajua? Hakuna mipaka kwa somo la “kumpenda Mungu.”

Na je, kuhusu ufahamu wa maisha ya mwanadamu ndani ya watu wote? Mtazamo wao kwa kumpenda Mungu ni upi? Wako radhi au hawako radhi? Je, wao hufuata halaiki kubwa, au huchukia sana mwili? Haya yote ni mambo mnayopaswa kuelewa kuyahusu na kuyafahamu, Je, kwa kweli hakuna chochote ndani ya watu? “Nataka mwanadamu anipende kweli, lakini leo, watu bado wanasitasita, wasiweze kunipa upendo wao wa kweli. Katika mawazo yao, wao huamini kwamba iwapo watanipa upendo wao wa kweli, wataachwa bila chochote.” Katika maneno haya, “upendo wa kweli” hasa una maana gani? Kwa nini Mungu bado anataka upendo wa kweli wa watu katika enzi hii wakati “watu wote wanampenda Mungu”? Hivyo, kusudi la Mungu ni kumtaka mwanadamu aandike maana ya upendo wa kweli juu ya karatasi ya majibu, na kwa hiyo, haya hasa ni matayarisho ambayo Mungu amempangia mwanadamu. Kuhusu hatua hii ya leo, hata ingawa Mungu hafanyi madai makuu kwa mwanadamu, watu bado hawajafikia matakwa ya Mungu ya asili kwa mwanadamu; kwa maneno mengine, bado hawajaweka nguvu zao zote katika kumpenda Mungu. Hivyo, katikati ya kutokuwa radhi kwao, Mungu bado anatoa matakwa Yake kwa watu, mpaka wakati kazi hii imekuwa na matokeo, na Yeye kutukuzwa katika kazi hii. Kweli, kazi iliyo duniani inahitimishwa kwa upendo kwa Mungu. Hivyo, wakati ambapo Mungu anahitimisha kazi Yake tu ndipo Anaashiria kazi muhimu zaidi ya wanadamu wote. Kama, wakati ambapo kazi Yake itaisha, atampa mwanadamu kifo, nini kitamfanyikia mwanadamu, nini kitamfanyikia Mungu, na nini kitamfanyikia Shetani? Ni wakati ambapo upendo wa Mungu duniani unashawishiwa ndio inaweza kusemekana kwamba “Mungu amemshinda mwanadamu.” La sivyo, watu wangesema kwamba Mungu humdhulumu mwanadamu, na Mungu angeaibishwa hivyo. Mungu hangekuwa mjinga hivyo kuihitimisha kazi Yake bila mnong’ono. Hivyo, wakati ambapo kazi inakaribia kuisha, shauku ya upendo wa Mungu hutokea, na upendo wa Mungu hugeuka kuwa mada motomoto. Bila shaka, huu upendo wa Mungu haujatiwa mawaa na mwanadamu, ni upendo usio ghushiwa, kama upendo wa mke mwaminifu kwa mme wake, au upendo wa Petro. Mungu hataki upendo wa Ayubu na Paulo, bali upendo wa Yesu kwa Yehova, upendo kati ya Baba na Mwana: “kufikiria tu kuhusu Baba, bila uzingatiaji wa hasara na faida za mtu binafsi, kumpenda tu Baba, na sio mwingine, na kutotaka kingine chochote.” Je, mwanadamu anaweza hili?

Tukilinganisha kile ambacho Yesu alifanya, Yule ambaye Hakuwa na ubinadamu kamili, tunaonaje? Mmefika umbali gani katika ubinadamu wenu kamili? Je, mnaweza kufikia sehemu moja kwa kumi ya kile Yesu alifanya? Mna sifa zinazostahili kwenda msalabani kwa ajili ya Mungu? Je, upendo wenu kwa Mungu unaweza kumwaibisha Shetani? Na mmetoa kiasi gani cha upendo wenu wa mwanadamu? Je, umebadilishwa na upendo wa Mungu? Ninyi hustahamili yote kwa kweli kwa ajili ya upendo kwa Mungu? Hebu fikirini kuhusu Petro wa nyakati zilizopita, na mjitazame, ninyi ambao ni wa leo—kuna tofauti kubwa kwa kweli, hamstahili

kusimama mbele ya Mungu. Ndani yenu, je, kuna upendo zaidi kwa Mungu, au upendo zaidi kwa ibilisi? Huu unapaswa kuwekwa kwa zamu upande wa kushoto na kulia wa mizani ya kupimia, kuona ni upi uko juu zaidi—je, kiasi gani cha upendo kwa Mungu kiko ndani yenu kwa kweli? Je, ninyi ni wa kufaa kufa mbele ya Mungu? Sababu ya Yesu kuweza kubaki msalabani ilikuwa kwa sababu uzoefu wake duniani ulitosha kumwaibisha Shetani, na ni kwa sababu hiyo tu ndiyo Mungu Baba alimruhusu kwa ujasiri kukamilisha hatua hiyo ya kazi; ilikuwa kwa ajili ya taabu Alizokuwa Amepitia na upendo Wake kwa Mungu. Lakini hamna sifa za kustahili jinsi hiyo. Hivyo, lazima mwendelee kupitia, kutimiza kuwa na Mungu, na si kingine chochote, ndani ya mioyo yenu—je, mnaweza kufanikisha hili? Kutokana na hili, inaweza kuonekana unamchukia Mungu kiasi gani, na unampenda Mungu kiasi gani. Si kwamba Mungu anataka mengi sana kwa mwanadamu, lakini kwamba mwanadamu hafanyi kazi kwa bidii. Je, hiki sicho kinachoendelea kwa kweli? La sivyo, ungegundua ndani ya Mungu kiasi gani kilicho cha kupendeza, na ungepata ndani yako kiasi gani kilicho cha kuchukiza sana? Unapaswa kufikiria kwa makini kuhusu mambo haya. Ni haki kusema kwamba ni wachache tu chini ya mbingu wanampenda Mungu—lakini unaweza kuwa mtangulizi, kuvunja rekodi ya dunia, na kumpenda Mungu? Mungu hataki chochote kutoka kwa mwanadamu. Mbona mwanadamu asimheshimu kwa hili? Je, huwezi kutimiza hata hili? Kuna nini lingine la kusema?

Sura ya 46

Miongoni mwa maneno haya yote, hakuna yasiyoweza kusahaulika zaidi kama yale ya leo. Awali maneno ya Mungu yalifichua hali za mwanadamu au siri za mbinguni, lakini tamko hili halifanani na yale ya wakati uliopita. Halidhihaki wala kufanya mzaha, lakini ni kitu kisichotarajiwa kabisa: Mungu aliketi chini na Akazungumza na watu kwa utulivu. Kusudi Lake ni gani? Unaona nini Mungu anaposema, “Leo, Nimeanza kazi mpya juu ya ulimwengu. Nimewapa watu walio duniani mwanzo mpya, na Nimewaambia wote watoke nyumbani Mwangu. Na kwa kuwa kila mara watu hupenda kujideka, Nawashauri wajijue, na wasiisumbue kazi Yangu kila mara”? Ni huu “mwanzo mpya” ambao Mungu anazungumzia ni upi? Hapo awali Mungu alishawashauri watu waondoke, lakini kusudi la Mungu wakati huo lilikuwa kupima imani yao. Kwa hiyo leo, Anaponena na sauti tofauti—Anakuwa halisi au mwongo? Awali, watu hawakujua Mungu alikuwa Akizungumza kuhusu majaribio gani. Ilikuwa tu kupitia hatua ya kazi ya watendaji-huduma ndipo macho yao yaliona, na wakapitia binafsi majaribio ya Mungu. Hivyo, tangu wakati huo na kuendelea, kwa msaada wa mifano ya mamia ya majaribio ya Petro, mara nyingi watu walifanya kosa la kuamini kwamba “Yalikuwa majaribio ya Mungu.” Zaidi ya hayo, katika maneno ya Mungu ukweli ulijitokeza lakini kwa nadra. Kwa hivyo, watu walizama zaidi kwa imani pofu kuhusu majaribio ya Mungu, na kwa hiyo katika maneno yote yaliyonenwa na Mungu, hawakuliamini hili kuwa kazi ya ukweli uliotekelezwa na Mungu;

badala yake, waliamini kwamba Mungu, kwa sababu hakuwa na lingine la kufanya, Alikuwa hasa Anatumia maneno kuwapima watu. Ilikuwa katikati ya majaribio kama hayo, ambayo hayakuwa na tumaini lakini yalionekana kuleta tumaini, ndipo watu walifuata, na kwa hiyo Mungu aliposema “wote ambao watabaki wataelekea kupitia msiba na ukosefu kidogo mwishowe.” watu bado walijitolea kuzingatia kufuata, na hivyo hawakuwa na nia ya kuondoka. Watu walifuata katikati ya njozi kama hizo, na hakuna hata mmoja wao aliyethubutu kuwa na hakika kwamba hakukuwa na tumaini—ambayo ni sehemu ya thibitisho la ushindi wa Mungu. Mtazamo wa Mungu unaonyesha kwamba Yeye hukishawishi kila kitu kimhudumie. Njozi za watu huwahimiza kutomwacha Mungu, bila kujali wakati au mahali, na kwa hiyo wakati wa hatua hii Mungu hutumia motisha za watu zenye dosari kuwafanya wawe na ushuhuda Kwake, ambao ni umuhimu mkuu wa wakati ambao Mungu asema, “Nimepata sehemu ya watu.” Shetani hutumia motisha za mwanadamu kusababisha ghasia, ilhali Mungu hutumia motisha za mwanadamu kumfanya ahudumu—ambayo ni maana halisi ya maneno ya Mungu kwamba “Wanafikiri kwamba wanaweza kuingia ndani kwa hila, lakini wanaponipa pasi zao za kuingia zisizo halisi, Nazitupa ndani ya shimo la moto papo hapo—na, wanapooni juhudi zao za kujitahidi’ zikiteketea moto, wanakata tamaa.” Mungu huvishawishi vitu vyote kuvifanya vihudumu, na kwa hiyo Haepuki maoni mbalimbali ya mwanadamu, bali huwaambia watu kwa ujasiri waondoke; hii ndiyo ajabu na hekima ya kazi ya Mungu, ikichanganya maneno ya kweli na mbinu kuwa kitu kimoja, ikiwaacha watu wakiwa wenye kuchanganyikiwa na waliokanganywa. Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba Mungu kweli anawataka watu watoke nyumbani Kwake, kwamba haya si aina fulani ya majaribio, na Mungu anachukua nafasi hii kusema, “Hata hivyo Mimi pia huwaambia watu kwamba wanapokosa kupata baraka, mtu yeyote asilalamike kunihusu.” Hakuna anayeweza kuelewa kama maneno ya Mungu ni halisi au ya uwongo, lakini Mungu hutumia nafasi hii kuwaimarisha watu, kuwanyang’anya hamu yao ya kuondoka. Hivyo, kama siku moja watalaaniwa, watakuwa wameonywa mapema kwa maneno ya Mungu, kama wasemavyo watu kwamba “maneno yasiyopendeza kusikia ndiyo mema.” Leo, upendo wa watu kwa Mungu ni wenye ari na wa kweli, na kwa hiyo katika maneno ambayo hawangeweza kufahamu kama yalikuwa halisi au ya uwongo, walishindwa na wakaja kumpenda Mungu, ndiyo maana Mungu alisema “Tayari nimefanikisha kazi Yangu kuu.” Mungu anaposema “Natumaini watapata njia yao wenyewe ya kuendelea kuishi. Mimi sina mamlaka katika hili,” huu ni uhalisi wa tamko la Mungu kuhusu maneno haya yote—hata hivyo watu hawafikiri hivyo; badala yake, kila mara wamefuata bila kutilia maanani maneno ya Mungu hata kidogo. Kwa hivyo, Mungu anaposema, “katika siku za baadaye, hakutakuwa tena na maneno yoyote kati yetu, hatutakuwa tena na jambo la kuzungumzia, hatutaingiliana, kila mmoja wetu atashika njia yake,” maneno haya ni ukweli, na hayajatiwa doa hata kidogo. Chochote ambacho watu hufikiria, hivyo ndivyo “kutokuwa na urazini” kwa Mungu kulivyo. Tayari Mungu

amekuwa na ushuhuda mbele ya Shetani, na Mungu alisema kwamba Atawafanya watu wote wasimwache haijalishi wakati au mahali—kwa hivyo hatua hii ya kazi imeshakamilishwa, na Mungu hayasikilizi malalamiko ya mwanadamu. Hata hivyo Mungu amelifafanua hili tangu mwanzo, kwa hivyo watu wanaachwa wakiwa wadhaifu, wanalazimika kuomba radhi. Vita kati ya Mungu na Shetani vinategemea mwanadamu kikamilifu. Watu hawawezi kujidhibiti, wao ni makaragosi kweli, huku Mungu na Shetani ndio wanaovuta kamba bila kuonekana. Mungu anapowatumia watu kuwa na ushuhuda Kwake, Yeye hufanya kila Awezalo kufikiri, Hufanya chochote kiwezekanacho, kuwatumia watu kumfanyia huduma, Akiwasababisha watu kutawaliwa na Shetani, na, zaidi ya hayo, kuongozwa na Mungu. Na wakati ambapo ushuhuda ambao Mungu anataka utolewe umemalizika, Yeye huwata watu upande mmoja na kuwaacha wakiteseka, huku Mungu anajifanya kwamba Hana shughuli nao. Wakati ambapo Anataka tena kuwatumia watu, Yeye huwaokota kwa mara nyingine na kuwatumia—na watu hawana ufahamu wa hili hata kidogo. Wao ni kama tu ng’ombe au farasi anayetumiwa jinsi atakavyo bwana wake, hakuna kati yao aliye na mamlaka juu yake mwenyewe. Hili linaweza kuonekana kuwa la kusikitisha kidogo, lakini haijalishi kama watu wana mamlaka juu yao wenyewe au la, kumfanyia Mungu huduma ni heshima, si kitu cha kumfadhaisha mtu. Ni kana kwamba Mungu anapaswa kutenda hivi. Je, kuweza kuridhisha hitaji la Mwenye Uweza si jambo la kujivunia? Kwa hiyo unaonaje? Je, umewahi kufanya azimio lako kutoa huduma kwa Mungu? Yawezekana kwamba bado unataka kushikilia haki yako ya kutafuta uhuru wako mwenyewe?

Hata hivyo, yote afanyayo Mungu ni mazuri, na yanastahili kuigwa, na mwanadamu na Mungu ni, hata hivyo, tofauti. Kwa msingi huu, unapaswa kumpenda Mungu kwa moyo wa utu bila kujali kama Mungu anastahi upendo wako au la. Maneno ya Mungu yanaonyesha kwamba pia kuna huzuni nyingi ndani ya moyo wa Mungu. Ni kwa ajili ya maneno ya Mungu tu ndio watu wanasafishwa. Lakini kazi hii, hata hivyo, ilifanyika jana—na kwa hiyo ni nini hasa ambacho Mungu atafanya kufuatia? Mpaka sasa, hii inabaki kuwa siri, na hivyo watu hawana uwezo wa kuelewea au kuifahamu, na wanaweza tu kufuata mkondo wa Mungu. Hata hivyo, yote ambayo Mungu asema ni kweli, yote hutimia—hili halina shaka!

Sehemu ya Tatu

Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani

(Juni 1992 hadi Agosti 2014)

Utangulizi

Sehemu hii ya maneno ya Mungu ina jumla ya vifungu vinne; vilionyeshwa na Kristo kati ya Juni ya 1992 na Septemba ya 2005. Nyingi zao zimetegemezwa kwa rekodi za mahubiri na

ushirika wa Kristo alipokuwa Akitembea miongoni mwa makanisa. Hazijabadilishwa kwa namna yoyote, wala hazijageuzwa baadaye na Kristo. Sehemu zilizobaki ziliandikwa na Kristo binafsi (Kristo anapoandika, Anafanya hivyo katika kikao kimoja, bila kusita ili kufikiria ama kufanya uhariri wowote, na maneno Yake ni maonyesho ya Roho Mtakatifu kikamilifu—hili ni jambo la hakika). Badala ya kutenganisha hizi aina mbili za matamshi, tumeziwasilisha pamoja, tukitumia mpangilio wa asili ambao ulitumiwa kuzionyesha; hili linatuwezesha kuona hatua za kazi ya Mungu kutoka kwa matamshi Yake yote, na kuelewa jinsi Anavyofanya kazi wakati wa kila awamu, jambo ambalo linafaidi ufahamu wa watu wa hatua za kazi ya Mungu na maarifa ya Mungu.

Sura nane za kwanza za “Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani I”—zinazojulikana kwa jumla kama “Njia”—ni sehemu ndogo ya maneno yaliyonenwa na Kristo alipokuwa sawa na mwanadamu. Licha ya jinsi zinavyoonekana kukosa ladha, zimejaa upendo na kujali kwa Mungu kuhusu wanadamu. Kabla ya hili, Mungu alizungumza kutoka kwa mtazamo wa mbingu ya tatu, jambo lililosababisha utengano mkubwa kati Yake na mwanadamu, na kuwafanya watu waogope kumkaribia Mungu, sembuse kumwomba Ayaruzuku maisha yao. Kwa hivyo, katika “Njia”, Mungu alimzungumzia mwanadamu kama aliyelingana naye na kuonyesha mwelekeo wa njia, hivyo kurejesha uhusiano wa mwanadamu na Mungu katika hali yake ya asili; watu hawakushuku tena iwapo Mungu bado alikuwa akitumia mbinu ya kuzungumza, na hawakusumbuliwa tena na hofu kuu ya jaribio la kifo. Mungu alishuka kutoka mbingu ya tatu hadi duniani, watu wakaja mbele ya kiti cha enzi cha Mungu kutoka katika ziwa la moto na kiberiti, wakatupilia mbali kivuli cha “watendaji huduma,” na kama ndama waliozaliwa karibuni, wakakubali kirasmi ubatizo wa maneno ya Mungu. Ni hapo tu ndipo Mungu aliweza kuzungumza nao waziwazi na kufanya kazi zaidi ya kuwapa uzima. Lengo la Mungu kujinyenyekeza kama mtu lilikuwa ili Awakaribie watu zaidi, hivyo kupunguza utengano kati yao na Yeye, na kumwezesha Apate utambuzi na imani ya watu, na kuwatia watu moyo wasadiki kufuatilia uzima na kumfuata Mungu. Sura nane za “Njia” zinaweza kufupishwa kama funguo ambazo Mungu hutumia kufungua milango ya mioyo ya watu, na kwa pamoja zinaunda tembe inayovutia ambayo Anampa mwanadamu. Mungu anapofanya hili tu ndipo watu wanaweza kutilia maanani mafundisho na makaripio ambayo Yeye hurudiarudia. Inaweza kusemekana kwamba ilikuwa tu baada ya hapa ndiyo Mungu alianza kirasmi kazi ya kutoa uzima na kuonyesha ukweli katika hatua hii ya sasa ya kazi, Alipokuwa akiendelea kuzungumza: “Maoni Wanayopaswa Kushikilia Waumini” na “Kwenye Hatua za Kazi ya Mungu”.... Je, mbinu kama hii haionyeshi maarifa ya Mungu na makusudi Yake ya ari? Huu ndio mwanzo kabisa wa Mungu kutoa uzima, kwa hiyo ukweli huu ni wa juujuu kiasi kuliko sehemu zinazofuata. Kanuni ya hili ni rahisi sana: Mungu hufanya kazi kulingana na mahitaji ya

wanadamu. Hatendi wala kuzungumza bila kufikiri; ni Mungu pekee anayeelewa mahitaji ya wanadamu kikamilifu, na hakuna mwingine anayempenda na kumfahamu mwanadamu zaidi.

Katika tamko la kwanza hadi tamko la kumi katika “Kazi na Kuingia,” maneno ya Mungu yanaingia katika awamu mpya. Matokeo yake ni kwamba matamshi haya yanawekwa mwanzoni. Kisha, “Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Mekanisani II” ilitokea. Wakati wa awamu hii, Mungu aliwatolea wafuasi Wake matakwa ya utondoti zaidi, matakwa yaliyojumuisha ufahamu kuhusu mitindo ya maisha ya watu, kinachohitajika kutoka kwa ubora wao wa tabia, na kadhalika. Kwa sababu watu hawa walikuwa wameazimia kumfuata Mungu, na hawakuwa tena na shaka kuhusu utambulisho na asili ya Mungu, Mungu pia alianza kirasmi kuwachukulia kama washirika wa familia Yake mwenyewe, Akishiriki ukweli wa ndani wa kazi ya Mungu kutoka wakati wa uumbaji hadi leo, Akifichua ukweli wa Biblia, na kuwafunza maana ya kweli ya Mungu kupata mwili. Matamshi ya Mungu katika sehemu hii yaliwapa watu ufahamu mzuri zaidi wa asili ya Mungu na asili ya kazi Yake, na yakawawezesha kutambua vyema kwamba kile walichopata kutoka kwa wokovu wa Mungu kilipita kile ambacho manabii na mitume walipata katika enzi zote zilizopita. Kutoka kwa kila mstari wa maneno ya Mungu, unaweza kuona busara Yake yote, na vilevile upendo mwadilifu na kumjali Kwake mwanadamu. Kando na kuonyesha maneno hayo, moja baada ya nyingine Mungu alifichua hadharani fikira na makosa ya awali ya mwanadamu na mambo ambayo watu hawakuwa wamewahi kufikiri, na pia njia ambayo watu walipaswa kuitembea baadaye. Huenda hili hasa ndilo “upendo” mdogo ambao mwanadamu anaweza kupitia! Hata hivyo, Mungu alikuwa amewapa watu yote waliyohitaji, na alikuwa amewapa kile walichotaka, bila kuzuia chochote ama kutaka kulipwa.

Sura kadhaa maalumu katika fungu hili zinazungumzia Biblia. Biblia imekuwa sehemu ya historia ya binadamu kwa miaka mingi. Zaidi ya hayo, watu huichukulia kuwa Mungu, kufikia kiwango ambapo katika siku za mwisho, imechukua nafasi ya Mungu, jambo ambalo linamchukiza Mungu. Hivyo, muda uliporuhusu, Mungu alihisi kulazimishwa kubainisha maelezo ya ndani na vyanzo vya Biblia; Asingefanya hivi, Biblia ingeendelea kushikilia nafasi ya Mungu mioyoni mwa watu, na watu wangetumia maneno ya Biblia kupima na kushutumu matendo ya Mungu. Kwa kuelezea asili, muundo na dosari za Biblia, Mungu hakuwa akikana kuwepo kwa Biblia hata kidogo, wala Hakuwa anaishutumu; badala yake, Alikuwa akitoa maelezo yaliyofaa na kustahili yaliyorejesha picha asilia ya Biblia, Akazungumzia suitafahamu za watu kuhusu Biblia, na kuwapa maoni sahihi ya Biblia, ili wasiabadu Biblia tena, na wasipotee tena; yaani, ili wasichanganye tena imani yao pofu ya Biblia kuwa imani katika Mungu na ibada ya Mungu, wakihofia hata kukabili usuli na dosari zake za kweli. Mara tu watu wanapopata ufahamu wa Biblia usiochanganywa na mambo duni, wanaweza kuiweka kando bila majuto na kuyakubali maneno mapya ya Mungu kwa ujasiri. Hili ndilo lengo la Mungu katika

sura hizi kadhaa. Ukweli ambao Mungu angetaka kuwaambia watu hapa ni kwamba hakuna nadharia ama ukweli ambao unaweza kuchukua nafasi ya kazi na maneno ya Mungu ya leo, na kwamba hakuna kitu kinachoweza kuwa mbadala wa Mungu. Ikiwa watu hawawezi kuepuka mtego wa Biblia, hawatawahi kuweza kuja mbele za Mungu. Ikiwa wanataka kuja mbele za Mungu, lazima kwanza waitakase mioyo yao na kuondoa chochote kinachoweza kuchukua nafasi Yake; kisha watamridhisha Mungu. Ingawa Mungu anaifafanua Biblia pekee hapa, usisahau kwamba kuna mambo mengi yenye makosa ambayo watu wanayaabudu kwa kweli kando na Biblia; mambo wasiyoyaabudu ni yale yanayotoka kwa Mungu kwa kweli pekee. Mungu anatumia tu Biblia kama mfano kuwakumbusha watu wasichukue njia mbaya, na wasivuke mipaka tena na kukanganyikiwa wanapomwamini Mungu na kukubali maneno Yake.

Maneno ambayo Mungu anampa mwanadamu yanageuka kutoka kuwa ya juujuu hadi kuwa ya kina. Mada za matamshi Yake husonga kutoka kwa tabia na matendo ya nje ya watu kuelekea tabia zao potovu, ambapo Mungu hutumia lugha Yake kulenga vina vya nafsi za watu: asili yao. Katika kipindi ambapo “Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani III” yalinenwa, matamshi ya Mungu yanasisitiza Asili na Utambulisho wa Mwanadamu, na maana ya kuwa mtu halisi—ukweli huu wa kina na maswali muhimu kuhusu watu kuingia katika uzima. Bila shaka, tukikumbuka ukweli ambao Mungu humpa mwanadamu katika “Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani I,” kwa kulinganishwa maudhui ya “Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani III,” ni ya kina sana. Maneno katika sehemu hii yanagusia njia ya watu ya baadaye na jinsi wanavyoweza kukamilishwa; pia yanagusia hatima ya baadaye ya wanadamu, na jinsi Mungu na mwanadamu wataingia pumzikoni pamoja. (Inaweza kusemekana kwamba hadi wa leo, haya ndiyo maneno ambayo Mungu amenena kwa watu kuhusu asili, misheni na hatima yao ambavyo ndivyo rahisi zaidi kuelewa.) Ni tumaini la Mungu kwamba watu wanaosoma maneno haya ni wale waliojitenga na fikira na mawazo ya binadamu, wanaoweza kufahamu vyema kila neno la Mungu kwa dhati. Aidha, Anatumai kwamba wale wote wanaoyasoma maneno haya wanaweza kuyachukulia maneno Yake kuwa ukweli, njia na uzima, na kwamba wasimtendee Mungu bila umakini ama kumrairai. Watu wakiyasoma maneno haya kwa mtazamo wa kumchunguza ama kumwangukia Mungu kwa makini, basi matamshi haya yatakuwa kama fumbo kwao. Ni wale tu wanaofuatilia ukweli, wanaodhamiria kumfuata Mungu, na wasio na shaka hata kidogo kumhusu ndio wanaostahili kuyakubali maneno haya.

“Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani IV” ni aina nyingine ya tamko takatifu inayofuata “Sehemu ya Pili Maneno ya Mungu kwa Ulimwengu Mzima.” Sehemu hii inajumuisha ushawishi, mafundisho na ufunuo wa Mungu kwa watu katika madhehebu ya Kikristo, kama vile: “Kufikia Utakapouona Mwili wa Kiroho wa Yesu, Mungu Atakuwa Ametengeneza Upya Mbingu na Dunia,” “Wale Ambao Hawalingani na Kristo Hakika Ni

Wapinzani wa Mungu.” Pia inajumuisha mahitaji maalum zaidi ya Mungu kwa wanadamu, kama vile: “Tayarisha Matendo Mema ya Kutosha kwa ajili ya Hatima Yako,” “Maonyo Matatu,” “Dhambi Zitamwelekeza Mwanadamu Jahanamu.” Vipengele vingi vimezungumziwa, kama vile ufunuo na hukumu ya watu wa aina zote na maneno kuhusu jinsi ya kumjua Mungu. Inaweza kusemekana kwamba fungu hili ndilo kiini cha Mungu kuwahukumu wanadamu. Sehemu isiyoweza kusahaulika kabisa ya fungu hili la matamshi ya Mungu ni kwamba, Mungu alipokuwa karibu kukamilisha kazi Yake, Alifichua kile kilicho katika asili ya watu: usaliti. Madhumuni Yake ni watu wajue ukweli ufuatao mwishowe kabisa, na kuacha ukite mizizi mioyoni mwao: Haijalishi umekuwa mfuasi wa Mungu kwa muda upi—asili yako bado ni kumsaliti Mungu. Yaani, ni asili ya mwanadamu kumsaliti Mungu, kwa sababu watu hawawezi kupevuka kabisa maishani mwao, na kunaweza tu kuwa na mabadiliko madogo katika tabia zao. Ingawa sura hizi mbili, “Usaliti (1)” na “Usaliti (2),” zinawashtua watu, kweli ni maonyo halisi na karimu zaidi ya Mungu kwa watu. Angalau kabisa, wakati watu wameridhika mno na ni wenye majivuno, baada ya kuzisoma sura hizi mbili, uovu wao wenyewe utazuiwa na watatulia. Kupitia sura hizi mbili, Mungu anawakumbusha watu wote kwamba bila kujali jinsi maisha yako yalivyoepvuka, jinsi uzoefu wako ulivyo wa kina, jinsi ujasiri wako ulivyo mkuu, bila kujali ulikozaliwa na unakoenda, asili yako ya kumsaliti Mungu inaweza kujifichua wakati wowote na mahali popote. Mungu anataka kumwambia kila mtu jambo hili: Ni asili ya kuzaliwa ya kila mtu kumsaliti Mungu. Bila shaka, nia ya Mungu ya kueleza sura hizi mbili si kupata sababu za kuwaondoa ama kuwashutumu wanadamu, ila ni kuwafanya watu wafahamu zaidi asili ya mwanadamu, ili waweze kuishi kwa uangalifu mbele za Mungu nyakati zote kupokea mwongozo Wake, jambo litakalowazuia kupoteza uwepo wa Mungu na kuingia kwenye njia mbaya. Hizi sura mbili ni onyo kwa wale wote wanaomfuata Mungu. Matumaini ni kwamba watu wataelewa nia za ari za Mungu; kwani maneno haya yote ni ukweli usioplingika—kwa hivyo mwanadamu ana haja gani ya kubishana kuhusu ni lini ama ni namna gani zilinenwa na Mungu? Ikiwa Mungu angejiwekea haya mambo yote, na Asubiri hadi watu walipoona wakati ulifaa wa Yeye kuzinena, muda haungekuwa umepita sana? Wakati huo unaofaa zaidi ungekuwa upi?

Mungu hutumia mbinu na mitazamo mingi katika hizi sehemu nne. Kwa mfano, wakati mwingine Anatumia tashtiti, na wakati mwingine Anatumia mbinu ya ruzuku na mafundisho ya moja kwa moja; wakati mwingine Anatumia mifano, na wakati mwingine Anatumia makaripio makali. Kwa jumla, kuna mbinu tofauti za kila aina, na lengo la mbinu hizi ni kuridhisha hali na mapendeleo mbalimbali ya watu. Mtazamo Anaotumia kuzungumza unabadilika kulingana na mbinu na maudhui tofauti ya matamshi Yake. Kwa mfano, wakati mwingine Anasema “Mimi”; yaani, Anawazungumzia watu kutoka kwa mtazamo wa Mungu Mwenyewe. Wakati mwingine Anazungumza kutoka kwa nafsi ya tatu, Akisema “Mungu” ni hili ama lile, na kuna nyakati

nyingine Anapozungumza kutoka kwa mtazamo wa mwanadamu. Bila kujali mtazamo Anaозungumza kutoka, asili Yake haibadiliki, kwani haijalishi Anavyozungumza, kila kitu Anachonena ni asili ya Mungu Mwenyewe—yote ni ukweli, na ndiyo ambayo wanadamu wanahitaji.

Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani I (Juni 1992 hadi Oktoba 1992)

Njia ... (1)

Katika maisha yake, hakuna mtu anayejua ni aina gani ya vipingamizi atakavyoenda kukutana navyo, wala hajui ni aina gani ya kusafishwa ambayo atapata mara kwa mara. Kwa wengine ni katika kazi yao, kwa wengine ni katika matazamio yao ya siku za baadaye, kwa wengine ni katika familia yao ya asili, na kwa wengine ni katika ndoa yao. Lakini kilicho tofauti nayo ni kwamba leo sisi, kundi hili la watu, tunateseka kwa ajili ya neno la Mungu. Yaani, kama mtu anayemtumikia Mungu, tumekumbana na vipingamizi katika njia ya kuamini katika Yeye, na hii ni njia ambayo waumini wote hufuata na ni njia iliyo chini ya miguu yetu yote. Ni kutoka katika kipengele hiki ndipo tunaanza rasmi mwendo wetu wa kuamini katika Mungu, kuanza maisha yetu kama binadamu, na kuingia katika njia sahihi ya maisha. Yaani, ni wakati ambapo tunaingia katika njia sahihi ya Mungu kuishi pamoja na mwanadamu, ambayo watu wa kawaida huifuata. Kama mtu anayesimama mbele ya Mungu na kumhudumia Yeye, yaani, mtu anayevaa mavazi rasmi ya kuhani katika hekalu, aliye na hadhi takatifu na mamlaka na uadhama wa Mungu, Natoa tangazo lifuatalo kwa watu wote. Kulieleza wazi zaidi: Sura tukufu ya Mungu ni utukufu Wangu, mpango wa usimamizi Wake ni kiini Changu. Sitafuti kupata mara mia katika ulimwengu ujao, lakini kuyafanya mapenzi ya Mungu katika ulimwengu huu ili Aweze kufurahia sehemu moja ndogo ya utukufu Wake duniani kwa ajili ya juhudi chache Ninazotoa katika mwili. Hii ndiyo shauku Yangu pekee. Katika maoni Yangu, hii ndiyo riziki Yangu ya pekee ya kiroho; Naamini kwamba haya yanapaswa kuwa “maneno ya mwisho” ya mtu anayeishi katika mwili na ambaye amejawa na hisia. Hii ni njia iliyo chini ya miguu Yangu leo. Naamini kwamba mtazamo huu Wangu ni maneno Yangu ya mwisho katika mwili, na natarajia kwamba watu hawana fikira au mawazo mengine kunihusu Mimi. Ingawa Nimejitoa kikamilifu, bado Sijaweza kuridhisha mapenzi ya Mungu mbinguni. Nina huzuni kupita kiasi—Mbona hiki ni kiini cha mwili? Kwa hiyo, kwa sababu ya mambo Niliyofanya katika siku zilizopita pamoja na kazi ya ushindi ambayo Mungu ametekeleza juu Yangu, ni wakati huu tu ndio Nimepata ufahamu wa kina wa kiini cha wanadamu. Ni tangu wakati huo tu ndipo Nimejiwekea Mwenyewe kiwango cha msingi zaidi: kutafuta tu kuyafanya mapenzi ya Mungu, kujitoa kikamilifu, na kutokuwa na chochote kinachosumbua dhamiri Yangu. Sijishughulishi na

masharti gani wengine wanaomhudumia Mungu wamejiwekea wenyewe. Kwa kifupi, Nimeutayarisha moyo Wangu kuyafanya mapenzi Yake. Hili ni ungamo Langu kama mmoja wa viumbe Wake anayehudumu mbele Yake—mtu ambaye ameokolewa na kupendwa na Mungu, na ambaye amevumilia mapigo Yake. Hili ni ungamo la mtu ambaye amelindwa, amehifadhiwa, amependwa, na kutumiwa sana na Mungu. Kuanza sasa na kuendelea, Nitaendelea katika njia hii mpaka Nimalize kazi muhimu iliyokabidhiwa Kwangu na Mungu. Lakini katika maoni yangu, mwisho wa safari uko karibu sana kwa sababu kazi Yake imetimizwa, na kufikia leo watu wamefanya yote wanayoweza kufanya.

Tangu wakati China bara ilipoingia katika mkondo huu wa kupata tena, makanisa yake ya mitaa yalikua polepole, yakiwa katikati ya kazi ya Roho Mtakatifu. Mungu amefanya kazi bila kukoma katika makanisa haya ya mitaa kwa sababu yamekuwa kiini cha Mungu katika familia ya kifalme iliyoanguka. Kwa sababu Mungu ameanzisha makanisa ya mitaa katika familia kama hizo, bila shaka yoyote Amejawa na furaha—ni furaha isiyo na kifani. Baada ya kuanzisha makanisa ya katika China bara na kueneza habari hii nzuri kwa ndugu katika makanisa mengine kote ulimwenguni, Mungu alisisimuka sana—hii ilikuwa hatua ya kwanza ya kazi Aliyotaka kufanya katika China bara. Ingesemwa kwamba hili lilikuwa tendo la kwanza, kwamba Mungu ameweza kuanza hatua ya kwanza ya kazi Yake katika mahali ambapo ni sawa na mji wa pepo wabaya usioshambuliwa na chochote, na mtu yeyote—je, hiyo si nguvu kuu ya Mungu? Ni wazi kwamba ili kupata tena kazi hii, ndugu wasiohesabika wameuawa kishahidi, wakifa kutokana na upanga wa mauaji wa shetani. Kulitaja hili wakati huu kunaleta huzuni nyingi, lakini kwa sehemu kubwa, siku za kuteseka zimepita. Sasa Naweza kumtumikia Mungu, na Nimeweza kufika mahali Nilipo leo yote ni kwa sababu ya nguvu za Mungu. Nina uvutiwaji mkuu kwa wale ambao Mungu aliwachagua kwa ajili ya kifo cha kishahidi—waliweza kuyafanya mapenzi ya Mungu na kujitoa wenyewe mhanga kwa ajili ya Mungu. Kusema kweli, kama isingekuwa kwa neema na fadhili za Mungu, Ngingekuwa nimezimia katika matope zamani sana. Shukrani ziwe kwa Mungu! Niko radhi kumpa Mungu utukufu wote, kumruhusu Yeye kuwa na raha. Watu wengine huniuliza Mimi: “Kwa sababu ya cheo chako Hupaswi kufa, kwa hivyo mbona Wewe hufurahi Mungu anapotaja kifo?” Huwa Sitoi jibu la moja kwa moja; Mimi huwapa tabasamu kidogo na kujibu: “Hii ni njia ambayo ni lazima Niifuatilie, ambayo ni lazima Niifuate bila shaka.” Watu huwa hawaelewi jibu Langu, lakini hunitazama Mimi kwa mshangao tu. Wao wanashangazwa kidogo Nami. Kwa hali yoyote, Naamini kwamba kwa vile hii ni njia ambayo Nimeichagua na pia ni uamuzi Nilioweka mbele ya Mungu, basi bila kujali shida zitakuwa kubwa vipi, Natia tu juhudi ili kuendelea kuifuata. Nafikiri kwamba hii ni ahadi inayopaswa kuungwa mkono na mtu anayemhudumia Mungu. Hawezi kuivunja ahadi yake hata kidogo. Hii pia ni amri, kanuni iliyotolewa zamani sana, katika Enzi ya Sheria, kwamba mtu anayeamini

katika Mungu anapaswa kufahamu. Katika uzoefu Wangu, maarifa yangu ya Mungu si makubwa na uzoefu Wangu wa utendaji si muhimu, hata hayastahili kutajwa, kwa hivyo siwezi kuzungumza kwa maoni yoyote ya fahari sana. Kwa hali yoyote, maneno ya Mungu ni lazima yaungwe mkono, na hayawezi kukaidiwa. Kusema kweli, uzoefu wa utendaji Wangu mwenyewe si mkubwa, lakini kwa sababu Mungu ana ushuhuda Kwangu na watu kila mara huwa na imani ya upofu katika mtu Niliye, Naweza kufanya nini? Bado Natarajia kwamba watu watarekebisha maoni yao juu ya kumpenda Mungu. Mtu Niliye si kitu, kwa vile Mimi pia Ninafuata njia ya imani katika Mungu, na njia Ninayoifuata si nyingine bali ni njia ya imani katika Mungu. Mtu ambaye ni mzuri hapaswi kuwa chombo cha kuabudu—anaweza tu kuwa mfano wa kuigwa. Sijali kile wanachofanya wengine, lakini Mimi huwatangazia watu kwamba Mimi pia humpa Mungu utukufu; Siupi mwili utukufu wa Roho. Natarajia kwamba kila mtu ataweza kuelewa hisia Zangu kuhusu hili. Sio kukwepa wajibu Wangu, lakini ni hadithi yote tu. Hili ni jambo ambalo linapaswa kuwa wazi kabisa, na kuanzia sasa halitahitaji kutajwa tena.

Leo, Nilitiwa nuru mbele ya Mungu. Kazi ya Mungu duniani ni kazi ya wokovu. Haina dosari na jambo lingine lolote. Watu wengine wanaweza kufikiria vingine, lakini Mimi huhisi kila mara kwamba Roho Mtakatifu anafanya tu hatua ya kazi ya wokovu, na sio kazi nyingine. Hili linapaswa kuwa wazi. Sasa tu ndipo kazi ya Roho Mtakatifu katika China bara imekuwa wazi. Na ni kwa nini Mungu angetaka kufungua njia zote na kufanya kazi mahali kama hapa, ambapo pepo wabaya wanakimbia na kutapakaa kila mahali? Inaweza kuonekana kutokana na hili kwamba kazi anayofanya Mungu kwa kiasi kikubwa ni kazi ya wokovu. Kuwa dhahiri kabisa, ni kwa kiasi kikubwa kazi ya ushindi. Kuanzia mwanzo jina la Yesu liliitwa. (Labda wengine hawajapitia hili, lakini Nasema kwamba hii ilikuwa hatua ya kazi ya Roho Mtakatifu.) Hili lilikuwa na makusudi ya kumwacha Yesu wa Enzi ya Neema, kwa hivyo sehemu ya watu walichaguliwa mapema, na kisha baadaye uteuzi huo ulifanywa kuwa mdogo. Baada ya hapo, jina la Witness Lee liliitwa katika China bara—hii ilikuwa sehemu ya pili ya kazi ya kupata tena ya Roho Mtakatifu katika China bara. Hii ilikuwa hatua ya kwanza ya kazi ambapo Roho Mtakatifu alianza kuwateua watu, ambayo ilikuwa kukusanya watu kwanza, kungoja mchungaji awatunze, na jina “Witness Lee” lilitumiwa kutenda huduma hiyo. Mungu binafsi alifanya kazi Yake baada ya kushuhudia jina “Mwenye Nguvu” na kabla ya hapo, ilikuwa katika hatua ya matayarisho. Kwa hivyo, haijalishi ikiwa hilo lilikuwa sahihi au baya, na sio suala kuu katika mpango wa Mungu. Baada ya kushuhudia jina “Mwenye Nguvu,” Mungu alianza rasmi kufanya kazi Yake binafsi na baada ya hilo, matendo Yake kama Mungu katika mwili yalianza rasmi. Kupitia jina “Bwana Mwenye Nguvu,” Aliwatawala wale wote waliokuwa waasi na wakaidi, na Wakaanza kuchukua ufanano wa binadamu, kama tu vile watu wanaanza kuonekana kama watu wazima wakati wanapohitimu ishirini na tatu au ishirini na nne; yaani, watu walikuwa tu

wameanza kuishi maisha ya binadamu wa kawaida, kupitia jaribio la watendaji huduma, kazi ya Mungu ilibadilika kwa kawaida kwa hatua ya kutenda kazi takatifu. Ingesemwa kwamba hatua hii ya kazi pekee ndiyo kiini cha kazi Yake nyingi na kwamba ni hatua ya msingi katika kazi Yake. Watu wanajijua na wanajichukia. Wamefikia mahali ambapo wanaweza kujilaani wenyewe, wanafurahia kusalimu amri maisha yao wenyewe na wana hisi hafifu ya kupendeza kwa Mungu. Ni juu ya msingi huu ndipo wanaelewa maana halisi ya maisha. Hii ni kutimiza mapenzi ya Mungu. Kazi ya Mungu katika China bara inakaribia mwisho. Mungu amekuwa akitekeleza matayarisho Yake katika nchi hii ya uchafu kwa miaka kadhaa, lakini watu hawakuwa wametimiza kiwango ambacho wamefikia sasa. Hii inamaanisha kwamba ni sasa tu ndio Mungu ameanza rasmi kazi Yake. Hakuna haja ya kutia utondoti au uwazi zaidi kuhusu hili. Ni sawa kabisa kusema kwamba kazi hii inafanywa moja kwa moja kupitia kwa utakatifu wa Mungu, lakini inatekelezwa kupitia kwa mwanadamu. Hakuna awezaye kukana hili. Kwa hakika ni kwa sababu ya nguvu kuu za Mungu duniani ndio kazi Yake ingefikia kiasi ambacho imefikia sasa katika watu wa nchi hii ya uasherati. Tunda la kazi hii lingepolekwa popote kuwaridhisha watu. Hakuna ambaye angethubutu kutoa hukumu kwa wepesi kuhusu hili na kulikana.

Njia ... (2)

Labda ndugu zetu wana muhtasari kidogo wa utaratibu, hatua, na mbinu za kazi ya Mungu katika China bara, lakini Mimi huhisi kila mara kwamba ni heri kuwa na kumbukumbu au muhtasari kidogo wa ndugu zetu. Ninatumia tu nafasi hii kusema machache ya kile kilicho moyoni Mwangu; Sizungumzi juu ya chochote nje ya kazi hii. Natarajia kwamba ndugu wanaweza kuelewa hali ya moyo Wangu, na pia Naomba kwa unyenyekevu kwamba wote wanaosoma maneno Yangu wafahamu na kusamehe kimo Changu kidogo, kwamba uzoefu Wangu wa maisha kweli si wa kutosha, na kwamba kweli Siwezi kuwa na ujasiri mbele ya Mungu. Kwa hali yoyote, Mimi huhisi kila mara kwamba hizi ni sababu halisi tu. Kwa kifupi, lolote litokealo, hakuna watu, matukio, au vitu vinavyoweza kuzuia ushirika wetu machoni pa Mungu, na Natarajia kwamba ndugu zetu wanaweza kufanya kazi kwa bidii zaidi mbele ya Mungu pamoja na Mimi. Ningependa kuomba ombi lifuatalo: “Ee Mungu! Tafadhali tuonyeshe fadhili ili Mimi na ndugu Zangu tuweze kujitahidi pamoja chini ya utawala wa maadili yetu ya pamoja, tuwe waaminifu Kwako hadi kifo, na tusiwahi kuvunja ahadi hii!” Maneno haya ni azimio Nililoweka mbele ya Mungu, lakini ingeweza pia kusemwa kwamba ni wito Wangu kama mwanadamu wa mwili anayetumiwa na Mungu. Nimeeleza hili mara nyingi katika ushirika pamoja na ndugu walio kandokando Yangu, na Nimetoa hili kama ujumbe kwa wale walio ubavuni Mwangu. Sijui watu wanalifikiria vipi, lakini bila kujali lolote litokealo, Naamini kwamba hawana tu hali ya juhudi za dhahania, lakini hata zaidi, pia wana hali ya nadharia halisi. Kwa sababu ya hili, inawezekana kwamba watu wengine wana maoni fulani, na unaweza

kuyachukua maneno haya kama wito wako na kuona jinsi msukumo wako wa kumpenda Mungu utakavyokuwa mkuu. Watu wengine watakuza fikira fulani watakaposoma maneno haya, na kufikiria: “Ni jinsi gani jambo hili la kusema kila siku, la kawaida linaweza kuwapa watu msukumo mkuu wa kumpenda Mungu hadi kifo? Na halina uhusiano wowote na mada ya kile tunachojadili, ‘Njia.’” Nakubali kwamba maneno haya hayana kiwango kikubwa sana cha uzuri, lakini Nimefikiria kila mara kwamba yanaweza kuwaongoza watu katika njia sahihi, na kuwaruhusu kupitia aina zote za majaribu kwa mwelekeo wa njia ya imani katika Mungu bila kukata tamaa au kurudi nyuma. Hii ndiyo maana kila mara Nauchukulia huu kuwa wito Wangu, na Natarajia kwamba watu wanaweza kufikiria juu ya hili kwa makini. Hata hivyo kusudi Langu si kumlazimisha kila mtu kukubali maoni Yangu—hili ni pendekezo tu. Bila kujali kile ambacho watu wengine wanafikiria kunihusu Mimi, Nafikiri kwamba Mungu atafahamu uwezo wa ndani wa kila mmoja wetu. Mungu daima anafanya kazi juu ya kila mmoja wetu, na kazi Yake ni isiyochoka. Hii ni kwa sababu sote tulizaliwa katika nchi ya joka kuu jekundu—hii ndiyo maana Anafanya kazi kwa njia hii ndani yetu. Wale waliozaliwa katika nchi ya joka kuu jekundu wana bahati kupata aina hii ya kazi ya Roho Mtakatifu. Kama mmoja wao, Nahisi sana pendo, heshima, pamoja na kupendeza kwa Mungu. Huyu ni Mungu anayetutunza. Ufalme ulio nyuma kimaendeleo, wenye kushikilia ukale, wa kikabaila, wa ushirikina, na wa upotovu wa tabaka la wafanyakazi kama huu hupata aina hii ya kazi kutoka kwa Mungu. Kutokana na hili, ni wazi kwamba sisi, kundi hili la watu katika enzi ya mwisho, tumebarikiwa sana. Naamini kwamba ndugu wote ambao macho yao ya kiroho yamefunguka kuiona kazi hii watalia machozi ya furaha kama matokeo. Na wakati huo, je, hutajionyesha kwa Mungu kwa kucheza na furaha? Je, hutamtolea Mungu wimbo ulio moyoni mwako? Wakati huo, je, hutaonyesha azimio lako kwa Mungu na kufanya mpango mwingine mbele Yake? Nafikiri kwamba yote haya ni mambo ambayo watu wa kawaida wanoamwamini Mungu wanapaswa kufanya. Kama wanadamu, Naamini kwamba kila mmoja wetu anapaswa kuwa na aina fulani ya maonyesho mbele ya Mungu. Hili ndilo mtu aliye na hisia anapaswa kufanya. Kwa kutazama uhodari wa kila mmoja miongoni mwetu na vilevile mahali petu pa kuzaliwa, inaonyesha kiwango cha aibu ambayo Mungu alivumilia ili kuja miongoni mwetu. Ingawa tuna maarifa fulani ya Mungu ndani yetu, kulingana na kile tunachojua, Mungu ni mkuu sana, mwenye uwezo mkubwa kabisa, na wa heshima sana, inatosha kujua jinsi mateso Yake yamekuwa makubwa miongoni mwa wanadamu kwa ulinganishi. Lakini hili bado ni jambo lisilo dhahiri kusema, na watu wanaweza tu kulichukulia kama maneno na mafundisho ya dini. Hii ni kwa sababu wale walio miongoni mwetu ni wasiosikia na wenye akili goigoi. Naweza tu kuongeza juhudi katika kueleza suala hili kwa wale ndugu wote ambao wangelikubali ili roho zetu ziweze kulisimuliwa na Roho wa Mungu. Mungu afungue macho yetu ya kiroho ili tuweze kuona gharama ambayo Mungu amelipa, juhudi ambazo Amefanya, na nguvu ambazo Ametumia kwa ajili yetu.

Kama mmoja wa wale walio katika China bara ambaye amekubali Roho wa Mungu, Nahisi kwa kina kwamba uhodari wetu unakosekana kweli. (Natarajia kwamba ndugu zetu hawatahisi vibaya kwa sababu ya hili—huu ni uhalisi wa hali.) Katika maisha Yangu ya utendaji Nimeona kwa dhahiri kwamba kile tunacho na tulicho yote ni yaliyo nyuma sana kimaendeleo. Katika hali kuu, ni jinsi tunavyotenda katika maisha yetu na uhusiano wetu na Mungu, na katika hali ndogo, ni kila wazo na fikira. Hivi vyote ni vitu vinavyoishi kwa uhalisi na ni vigumu kuficha kwa maneno au vitu vya uongo. Kwa hivyo, Nisemapo hili watu wengi huashiria kwa vichwa vyao na kulikubali, na wao huridhishwa nalo isipokuwa wawe ni watu wanaokosa mantiki ya kawaida. Mtu wa aina hiyo hawezi kukubali aina hii ya mtazamo Wangu. Labda sijui kwa kweli jinsi ya kuwa wa adabu, na Ninamtaja kwa waziwazi mtu wa aina hiyo kama mnyama kwa hakika. Hii ni kwa sababu mtu wa aina hiyo ni wa chini sana juu ya mti wa mzimu katika nchi ya joka kuu jekundu—yeye ni kama nguruwe au mbwa. Mtu wa aina hiyo amepungukiwa sana katika uhodari, na hastahili kuja mbele ya Mungu. Labda ni kwamba maneno Yangu ni ya kifidhuli sana. Kwa kumwakilisha Roho wa Mungu anayefanya kazi ndani Yangu, Mimi nalaani aina hii ya kiumbe aliye kama mnyama, mchafu, na Natarajia kwamba ndugu Zangu hawadhoo fishwi na hili. Inawezekana kwamba hatuna mtu wa aina hii miongoni mwetu, lakini bila kujali ukweli ni upi, Naamini kwamba hivi ndivyo mtu wa aina hiyo anapaswa kushughulikiwa. Unaonaje?

Miaka elfu kadhaa ya ufalme wa joka kuu jekundu umepotoshwa wakati huo wote mpaka sasa, na kwa sababu umepinga Mungu kwa uthabiti, Mungu ameilaani nchi hii na kuishughulikia kwa ghadhabu, na baada ya hilo Ameigawia kuadibu Kwake. Nchi hii iliyolaaniwa na Mungu imetawaliwa na utenganisho wa kimbari, na bado iko katika hali ya kuwa nyuma kimaendeleo. Nchi tuliyozaliwa ndani ni uwanja wa mkusanyiko wa pepo wabaya wengi, na kwa hivyo wanatapakaa kote na kutafuta kutawala katika nchi hii. Hili limesababisha kuchafuliwa kwa wale waliozaliwa hapa. Mienendo, mila, na mawazo na dhana za watu ni za nyuma kimaendeleo na za mtindo wa zamani, kwa hiyo zinaunda aina zote za fikira kuhusu Mungu ambazo kufikia sasa wameshindwa kuziondoa. Hasa, wao hutenda kwa njia moja mbele ya Mungu na kutenda kwa njia nyingine nyuma Yake, wakidhanja kumhifadhi Shetani ni kumhudumia Mungu. Hili ni onyesho la kuwa nyuma sana kimaendeleo. Mungu amefanya kazi nyingi sana katika China bara na Amenena maneno Yake mengi sana, lakini watu bado ni wasiosikia kabisa na wasiojali. Bado wanafanya kazi yao kama walivyofanya awali na hawana kabisa ufahamu wa maneno ya Mungu. Mungu alipotangaza kwamba hakukuwa na mategemeo na wala matumaini, kanisa lililokuwa hai na lenye joto la majira ya joto liliingia katika majira ya baridi. Nafsi halisi za watu zilifichuliwa katika nuru ya mchana na ujasiri, upendo, na nguvu zao za awali vyote vilitoweka bila dalili yoyote. Na sasa, hakuna aliyepata tena uchangamfu wake. Wanasema na maneno yao kwamba wanampenda Mungu, na ingawa hawathubutu kulalamika

katika mioyo yao, haijalishi chochote hawana upendo huo katu. Hilo linahusu nini? Nafikiri kwamba ndugu zetu wataukubali ukweli huu. Mungu atupe nuru, ili sote tuweze kujua kupendeza Kwake, kumpenda Mungu wetu katika kina cha mioyo yetu, na kuonyesha upendo ambao sote tunao kwa Mungu katika nafasi mbalimbali; Mungu atupe mioyo thabiti yenye upendo wa kweli Kwake—hili ndilo Ninalotarajia. Baada ya kusema hili, Nahisi huruma kidogo kwa ndugu Zangu waliozaliwa pia katika nchi hii ya uchafu, na kwa hiyo chuki yangu dhidi ya joka kuu jekundu imekua ndani yangu. Linazuia upendo wetu kwa Mungu na kushawishi ulafi wetu wa matazamio yetu ya baadaye. Linatushawishi kuwa wabaya, kumpinga Mungu. Limekuwa joka kuu jekundu ambalo limetudanganya, limetupotosha, na kutuangamiza mpaka sasa, kiasi kwamba hatuwezi kulipa upendo wa Mungu kwa mioyo yetu. Tuna msukumo ndani ya mioyo yetu lakini ijapokuwa sisi wenyewe, hatuna nguvu. Sisi sote ni waathiriwa. Kwa sababu hii, Nalichukia kutoka kwa kiini Changu na Siwezi kungoja kuliharibu. Kwa hali yoyote, Ninapofikiria tena, hili halingekuwa na mafanikio na lingelea tu tatizo kwa Mungu, kwa hiyo Narudi kwa maneno haya—Nimeamua kuyafanya Mapenzi Yake—kumpenda Mungu. Hii ndio njia Ninayofuata—ni njia ambayo Mimi, mmoja wa viumbe Wake, Napaswa kuitembea. Ni jinsi Napaswa kuishi maisha Yangu. Haya ni maneno kutoka moyoni Mwangu, na Natarajia kwamba ndugu Zangu watapata kutiwa moyo kwa kiasi fulani baada ya kuyasoma maneno haya ili moyo Wangu uweze kupata kiasi fulani cha amani. Kwa kuwa lengo Langu ni kuyafanya mapenzi ya Mungu na hivyo kuishi kwa kudhihirisha maisha yaliyojaa maana na mng'aro. Katika hili, Nitaweza kufa bila majuto, na moyo uliojaa furaha na faraja. Je, ungependa kufanya hilo? Wewe ni mtu aliye na aina hiyo ya azimio?

Kwamba Mungu anaweza kufanya kazi ndani ya wale wanaoitwa “Mtu Mgonjwa wa Asia Mashariki” ni nguvu Zake kuu. Ni unyenyekevu na kujificha Kwake. Bila kujali maneno Yake makali au kuadibu kunakoelekezwa kwetu, tunapaswa kumsifu Yeye kutoka ndani ya mioyo yetu kwa unyenyekevu Wake, na kumpenda Yeye mpaka mwisho kabisa wa hili. Watu ambao wamefungwa na Shetani kwa miaka elfu kadhaa wameendelea kuishi chini ya ushawishi wake na hawajamtupilia mbali. Wameendelea kupapasa na kupambana kwa uchungu. Zamani wangepukiza, na kumwinamia na kumhifadhi Shetani, na walikuwa wamefungwa kabisa kwa mitego ya familia na ya kidunia pamoja na maingiliano ya kijamii. Hawakuweza kuyatupilia mbali. Katika aina hii ya jamii ya unyang’au, ni wapi ambapo mtu anaweza kupata maisha ya maana? Kile ambacho watu husimulia ni maisha ya mateso, na kwa bahati nzuri, Mungu amewaokoa watu hawa wasio na hatia, na kuyaweka maisha yetu chini ya utunzaji Wake na ulinzi Wake ili maisha yetu yawe ya furaha na yasiyojaa tena wasiwasi. Tumeendelea kuishi chini ya neema Yake mpaka sasa. Je, hii si baraka ya Mungu? Mtu anawezaje kuthubutu kumdai Mungu kupita kiasi? Ametupa chache sana? Bado hamjaridhika? Nafikiri kuwa wakati

umewadia wa sisi kulipa upendo wa Mungu. Ingawa tutapata mara kwa mara dhihaka, kashfa, na mateso mengi sana kwa sababu tunafuata njia ya imani katika Mungu, Naamini hili ni jambo la maana. Ni jambo la utukufu, sio aibu, na lolote litokealo, baraka tunazofurahia si hafifu kamwe. Katika nyakati nyingi za masikitiko, maneno ya Mungu yameleta faraja, na kufumba na kufumbua, huzuni imegeuka na kuwa furaha. Katika nyakati nyingi za hitaji, Mungu ameleta baraka na tumekimiwa kupitia kwa maneno Yake. Katika nyakati nyingi za magonjwa, maneno ya Mungu yameleta uzima—tumewekwa huru kutoka kwa hatari, na kugeuka kutoka kwa hatari hadi kwa usalama. Tayari umefurahia vitu vingi kama hivi bila kutambua hilo. Inawezekana kwamba hukumbuki?

Njia ... (3)

Katika maisha Yangu, Niko radhi kila mara kujitolea Mwenyewe kwa Mungu kabisa, mwili na fikra. Kwa njia hii, hakuna lawama kwa dhamiri Yangu na Naweza kupata kiasi kidogo cha amani. Mtu anayeandama uzima ni lazima kwanza aukabidhi moyo wake wote kwa Mungu kabisa. Hili ni sharti la mwanzo. Ningependa ndugu Zangu wamwombe Mungu pamoja na Mimi: “Ee Mungu! Roho Wako aliye mbinguni awape neema watu walio duniani ili moyo Wangu uweze kukugeukia Wewe kikamilifu, kwamba Roho Yangu iweze kusionuliwa Nawe, na kwamba Niweze kuona kupendeza Kwako ndani ya moyo Wangu na Roho Yangu, ili wale walio duniani wabarikiwe kuuona uzuri Wako. Mungu! Roho Wako mara tena asisimue roho zetu ili upendo wetu uwe wa kudumu na usibadilike kamwe!” Kile ambacho Mungu hufanya ndani yetu sote ni kuijaribu mioyo yetu kwanza, na tunapomimina mioyo yetu ndani Yake, ni wakati huo ndipo Yeye huanza kusisimua roho zetu. Ni katika roho tu ndipo mtu anaweza kuona kupendeza, uwezo wa juu kabisa, na ukuu wa Mungu. Hii ni njia ya Roho Mtakatifu ndani ya wanadamu. Je, una maisha ya aina hii? Umepitia maisha ya Roho Mtakatifu? Roho yako imesisimuliwa na Mungu? Umeona jinsi ambavyo Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani ya watu? Umeukabidhi moyo wako kwa Mungu kabisa? Ukiukabidhi moyo wako kwa Mungu kikamilifu, unaweza kupitia moja kwa moja maisha ya Roho Mtakatifu, na kazi Yake inaweza kufichuliwa daima kwako. Wakati huo, unaweza kuwa mtu anayetumiwa na Roho Mtakatifu. Je, uko radhi kuwa mtu wa aina hiyo? Katika kumbukumbu Yangu, Niliposisimuliwa na Roho Mtakatifu na kumpa Mungu moyo Wangu mara ya kwanza, Nilianguka chini mbele Yake na kupaza sauti: “Ee Mungu! Ni Wewe uliyeyafungua macho Yangu ili Niweze kuelewa wokovu Wako. Niko radhi kukupa Wewe moyo Wangu kabisa, na kile Ninachoomba ni kwamba mapenzi Yako yafanyike. Kile Ninachotamani ni kwamba moyo Wangu upate kibali Chako machoni Pako, na kuyafanya mapenzi Yako.” Ombi hilo ndilo lisilosahaulika kamwe Kwangu; Nilisisimuliwa sana, na Nikalia kwa uchungu mbele ya Mungu. Hilo lilikuwa ombi Langu lililofanikiwa la kwanza mbele ya Mungu kama mtu ambaye ameokolewa, na ilikuwa hamu Yangu ya kwanza.

Nilisisimuliwa mara kwa mara na Roho Mtakatifu baada ya hilo. Umekuwa na aina hii ya tukio? Ni jinsi gani Roho Mtakatifu amefanyaje kazi ndani yako? Nafikiri kwamba watu wanaotafuta kumpenda Mungu wote watakuwa na aina hii ya tukio, kwa viwango vikubwa zaidi au vidogo zaidi, lakini watu huyasahau. Mtu akisema hajakuwa na aina hii ya tukio, hii inathibitisha kwamba bado hajaokolewa na bado yuko chini ya miliki ya Shetani. Kazi ambayo Roho Mtakatifu hutekeleza ndani ya kila mtu ni njia ya Roho Mtakatifu, na pia ni njia ya mtu anayemwamini na kumtafuta Mungu. Hatua ya kwanza ya kazi ambayo Roho Mtakatifu hutenda juu ya watu ni ile ya kuisimua roho zao. Baada ya hiyo, wataanza kumpenda Mungu na kufuatilia maisha; wale wote walio katika njia hii wako ndani ya mkondo wa Roho Mtakatifu. Huu sio uwezo tu wa kazi ya Mungu katika China bara, lakini pia katika ulimwengu mzima. Yeye hufanya hili juu ya wanadamu wote. Ikiwa mtu kamwe hajasisimuliwa hata mara moja tu, hii inathibitisha kwamba wao wako nje ya mkondo huu wa kupata tena. Moyoni mwangu, humwomba Mungu bila kikomo, nikiomba kwamba Atawasisimua watu wote, ili kwamba kila mtu chini ya jua asisimuliwe Naye na kutembea njia hii. Labda hili ni ombi ndogo sana Ninalomwomba Mungu, lakini Naamini kwamba Atatenda hili. Natarajia kwamba ndugu Zangu wote wataliombea hili, kwamba mapenzi ya Mungu yatendeke, na kwamba kazi Yake ihitimishwe hivi punde ili Roho Wake aliye mbinguni aweze kuwa na raha. Hili ni tarajio Langu dogo.

Naamini kwamba kwa vile Mungu anaweza kutekeleza kazi Yake katika mji mmoja wa pepo wabaya, basi Anaweza bila shaka kutekeleza kazi Yake katika miji mingi ya pepo wabaya kutoka upande mmoja hadi mwingine wa ulimwenguni. Sisi ambao ni wa enzi ya mwisho tutaona bila shaka siku ya utukufu wa Mungu. Hii inaitwa “kufuata hadi mwisho kutasababisha wokovu.” Hakuna anayeweza kumbadilisha Mungu katika hatua hii ya kazi Yake—ni Mungu Mwenyewe tu anaweza kufanya hivyo. Hii ni kwa sababu ni ya ajabu; ni hatua ya kazi ya ushindi, na wanadamu hawawezi kuwashinda wanadamu wengine. Ni maneno tu ya kutoka kinywani mwa Mungu na mambo Ayafanyayo binafsi ndiyo yanaweza kuwashinda wanadamu. Kutoka kwa ulimwengu mzima, Mungu anatumia nchi ya joka kuu jekundu kama uwanja wa majaribio, baada ya hapo, Atapakia kwa kazi hii kote ulimwenguni. Hiyo basi, atatekeleza hata kazi kubwa zaidi ulimwenguni kote, na watu wote wa ulimwengu watapokea kazi ya Mungu ya ushindi. Watu wa kila dini na kila dhehebu lazima wakubali hatua hii ya kazi. Hii ni njia ambayo ni lazima ifuatwe—hakuna anayeweza kuiepuka. Je, uko radhi kukubali hiki ulichoaminiwa na Mungu? Mimi huhisi kila mara kwamba kukubali kitu unachoaminiwa na Roho Mtakatifu ni jambo la utukufu. Vile Ninavyoona, hii ndiyo amana kuu sana ambayo Mungu huweka katika wanadamu. Natarajia kuwa na ndugu Zangu wakifanya kazi kwa bidii ubavuni Mwangi na kukubali hili kutoka kwa Mungu, ili Mungu atukuzwe kote kote katika ulimwengu, na katika

eneo la juu, na maisha yetu hayatakuwa bure. Tunapaswa kumfanyia Mungu kitu, au tunapaswa kula kiapo. Ikiwa mtu anaamini katika Mungu lakini hana kusudi la kufuatilia, basi maisha yake huwa kazi bure, na wakati ufikapo wa yeye kufa, wao wana anga la samawati na ardhi ya vumbi tu ya kutazama. Je, hayo ni maisha ya maana? Ikiwa unaweza kutimiza masharti ya Mungu ukiwa bado hai, hili si jambo zuri? Mbona kila mara unatafuta tatizo, na mwenye huzuni? Kwa njia hiyo unapata chochote kutoka kwa Mungu? Mungu anaweza kupata chochote kutoka kwako? Katika ahadi Niliyofanya na Mungu, Mimi nampa tu moyo Wangu na Simpumbazi kwa maneno Yangu. Singefanya kitu kama hicho—Mimi niko radhi tu kumfariji Mungu Nimpendaye kwa moyo Wangu, ili Roho Wake aliye mbinguni afarijiwe. Moyo unaweza kuwa na thamani lakini upendo una thamani kuu zaidi. Niko radhi kumtolea Mungu upendo wa thamani kubwa zaidi moyoni Mwangu ili kile Anachofurahia kiwe ni kitu kizuri zaidi Nilichonacho, ili Akamilishwe na upendo Ninaomtolea Yeye. Je, uko radhi kumpa Mungu upendo wako ili Afurahie? Je, uko radhi kuifanya hii kuwa raslimali yako wewe ya kuendelea kuishi? Ninachooni kutokana na uzoefu Wangu ni kwamba kadri Ninavyompa Mungu upendo mwingi, ndivyo Ninavyohisi kwamba Ninaishi kwa furaha, na Nina nguvu zisizo na mipaka, Niko radhi kutoa mwili na mawazo Yangu yote kama dhabihu, na kuhisi kila mara kwamba Siwezi kabisa kumpenda Mungu vya kutosha. Kwa hiyo je, upendo wako ni upendo usio muhimu, au ni usio na kikomo, wa kupita kiasi? Ikiwa kweli unataka kumpenda Mungu, utakuwa kila mara na upendo zaidi wa kumrudishia Yeye. Ikiwa hali ni hiyo, ni mtu gani na ni kitu gani kina uwezo wa kuzuia upendo wako kwa Mungu?

Mungu huona upendo wa wanadamu wote kuwa wa thamani; Yeye hulimbikiza baraka Zake nyingi zaidi juu ya wote wanaompenda Yeye. Hii ni kwa sababu upendo wa mwanadamu ni mgumu sana kupatikana, kunao kidogo sana, na nusura usiweze kupatikana. Kotekote ulimwenguni, Mungu amejaribu kudai kwamba watu warudishe upendo Kwake, lakini katika enzi zote mpaka sasa, wale ambao wametoa upendo halisi kwa Mungu ni wachache—ni wachache katika idadi. Kadri Ninavyokumbuka, Petro alikuwa mmoja, lakini aliongozwa binafsi na Yesu na ni wakati tu wa kifo chake ndipo alipompa Mungu upendo wake wote, kumaliza hayo maisha yake. Kwa hivyo, ni katika aina hizi za hali zisizofaa ndipo Mungu amefanya eneo la kazi Yake kuwa dogo katika ulimwengu, kwa kutumia nchi ya joka kuu jekundu kama eneo la maonyesho, Akielekeza nguvu Zake zote na juhudi Zake zote mahali pamoja, ili kuifanya kazi Yake kuwa ya ufanisi zaidi, na yenye manufaa makubwa kwa ushuhuda Wake. Ni katika hali hizi mbili ndipo Mungu alisongeza kazi Yake ya ulimwengu mzima kwa watu hawa wenye uhodari duni katika China bara na kuanza kazi Yake yenye upendo ya ushindi ili baada ya watu hawa kuweza kumpenda Yeye, Aweze kutekeleza hatua inayofuata ya kazi Yake. Huu ni mpango wa Mungu. Matunda ya kazi Yake yatakuwa makubwa zaidi kwa njia hii. Upeo wa kazi

Yake una msingi na udhaifu. Ni wazi kuhusu namna ya kiasi kukubwa cha gharama ambayo Mungu amelipa na kiasi cha juhudi ambazo Ametumia kwa kutekeleza kazi Yake ndani yetu, kwamba siku yetu imefika. Hii ni baraka yetu. Kwa hivyo, kile ambacho hakilingani na fikira za wanadamu ni kwamba wenyeji wa Magharibi hutuonea wivu kwa kuzaliwa mahali pazuri, lakini sisi wote hujiona kuwa duni na wanyonge. Je, huyu si Mungu anayetuinua? Uzao wa joka kuu jekundu ambao wamekuwa wakikandamizwa kila mara wanategemewa na wenyeji wa Magharibi—hii ni baraka yetu kweli. Ninapofikiria juu ya hili, Ninajawa na wema wa Mungu, na upendo na ukaribu Wake. Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba lile afanyalo Mungu ni kinyume cha fikira za wanadamu, na ingawa watu hawa wote wamelaaniwa, Hashurutishwi na shutuma za sheria na Amehamisha katikati kwa kudhamiria kazi Yake pande zote za kwa sehemu hii ya dunia. Hii ndio maana nafurahi, ndio maana nahisi furaha ya kupita kiasi. Kama mtu anayechukua wajibu wa kuongoza katika kazi hii, kama vile makuhani wakuu miongoni mwa Waisraeli, Ninaweza kutekeleza moja kwa moja kazi ya Roho na kuhudumia moja kwa moja Roho wa Mungu; hii ni baraka Yangu. Nani angethubutu kufikiria juu ya jambo kama hili? Lakini leo, hili limetujia sisi bila kutazamiwa. Ni furaha kuu kweli inayostahili sherehe yetu. Natarajia kwamba Mungu ataendelea kutubariki na kutuina ili sisi tulio katika lundo la samadi tutumiwe kwa kiwango kikubwa na Mungu, hivyo kuturuhusu kulipa upendo Wake.

Kulipa upendo wa Mungu ni njia ambayo Ninafuata sasa, lakini Nahisi kwamba haya si mapenzi ya Mungu, wala si njia Ninayopaswa kutembea. Mapenzi ya Mungu ni kuwa Mimi nitumiwe kwa kiwango kikubwa na Yeye—hii ni njia ya Roho Mtakatifu. Labda Nimekosea. Nafikiri hii ni njia Ninayofuata tangu Nilipoanzisha azimio Langu na Mungu kitambo sana. Niko radhi kumwacha Mungu aniongoze ili Niingie katika njia Ninayopaswa kuifuata mapema iwezekanavyo, na kuridhisha mapenzi ya Mungu mapema iwezekanavyo. Bila kujali kile ambacho wengine watafikiria, Naamini kwamba kuyafanya mapenzi ya Mungu ni la muhimu zaidi na ni jambo muhimu zaidi la maisha Yangu. Hakuna yeyote anayeweza kuninyang’anya Mimi haki hii—huu ni mtazamo Wangu binafsi, na labda kuna wengine ambao hawawezi kuufahamu, lakini naamini kwamba Sihitaji kuthibitisha uhalali wa hili kwa yeyote. Nitafuata njia Ninayopaswa kufuata—mara tu Nikitambua njia Ninayopaswa kuifuata Nitaifuata na Sitarudi nyuma. Hivyo Narudi kwa maneno haya: Nasababisha moyo Wangu kufanya mapenzi ya Mungu. Natazamia kwamba ndugu Zangu hawatanikosoa! Kwa jumla, Ninavyoona binafsi, watu wengine wanaweza kusema wanachopenda, lakini Nahisi kwamba kufanya mapenzi ya Mungu ni muhimu sana na Sipaswi kutii vizuizi kuhusu hili. Siwezi kukosea Ninapofanya mapenzi Yake, na kufanya hili hakuwezi kupangwa kulingana na upendeleo Wangu Mimi. Naamini kwamba Mungu ameona ndani ya moyo Wangu! Kwa hivyo ni jinsi gani unapaswa kufahamu hili? Uko radhi kujitolea mwenyewe kwa ajili ya Mungu? Uko radhi kutumiwa na

Mungu? Azimio lako wewe ni kufanya mapenzi ya Mungu? Natarajia kwamba ndugu Zangu wote wanaweza kupata msaada wa kiwango fulani kutoka kwa maneno Yangu. Ingawa maoni Yangu Mimi ni ya juujuu, bado Ninasema Ninachoweza kusema ili sote tuweze kuwa na mazungumzo ya wazi yasiyo na vizuizi, ili Mungu abaki miongoni mwetu milele. Haya ni maneno kutoka moyoni Mwangu. Sawa! Hayo ni yote kuhusu maneno Yangu ya dhati kwa leo. Natarajia kwamba ndugu Zangu wataendelea kufanya kazi kwa bidii, na Natarajia kwamba Roho wa Mungu atatutunza kila wakati!

Njia ... (4)

Kwamba watu wanaweza kugundua kupendeza kwa Mungu, kutafuta njia ya kumpenda Mungu katika enzi hii, na kwamba wako radhi kukubali mafunzo ya ufalme wa leo—hii yote ni neema ya Mungu na hata zaidi, ni Yeye ndiye anawainua wanadamu. Kila Nifikiriapo juu ya hili Mimi huhisi kwa uthabiti kupendeza kwa Mungu. Ni kweli kwamba Mungu anatupenda. La sivyo, nani angeweza kutambua kupendeza Kwake? Ni kutoka tu kwa hili ndio Naona kwamba kazi hii yote inafanywa binafsi na Mungu Mwenyewe, na watu wanaongozwa na kuelekezwa na Mungu. Natoa shukrani kwa Mungu kwa hili, na Ningependa ndugu na dada Zangu wajiunge na Mimi kumsifu Mungu: “Utukufu wote uwe Kwako, Mungu Mwenyewe mwenye uwezo mkubwa kabisa! Utukufu Wako uzidishwe na kufichuliwa ndani yetu sisi ambao tumeteuliwa na kupatwa na Wewe”. Nimepata nuru kutoka kwa Mungu—kabla ya enzi Mungu alikuwa tayari ametujaalia na Alitaka kutupata katika siku za mwisho, hivyo kuruhusu ulimwengu na vitu vyote kuona utukufu wa Mungu katika uzima wake kupitia kwetu. Hivyo, sisi ni dhihirisho la miaka elfu sita ya mpango wa usimamizi wa Mungu; sisi ni vielelezo, sampuli za kazi ya Mungu katika ulimwengu wote. Ni kufikia wakati huu tu ndio Nimeweza kugundua ni upendo wa kiasi gani alio nao Mungu kwa kweli kwetu, na kwamba kazi Afanyayo ndani yetu na mambo Ayasemayo yote yanapita yale ya enzi zilizopita mara milioni. Hata katika Israeli na ndani ya Petro, Mungu hakuwahi kufanya binafsi kazi nyingi hivyo na kuzungumza mengi hivyo. Hili linaonyesha kwamba, hili kundi la watu, kweli wamebarikiwa ajabu sana—limebarikiwa zaidi ya watakatifu wa nyakati zilizopita kwa kiasi kisichoweza kulinganishwa. Hii ndio maana Mungu amesema kila mara kwamba watu wa enzi ya mwisho wamebarikiwa. Haijalishi wengine wanasema nini, Naamini kwamba sisi ndio wale wamebarikiwa zaidi na Mungu. Tunapaswa kukubali baraka tulizopewa na Mungu; labda kuna wengine ambao watalalamika kwa Mungu, lakini Naamini kwamba baraka hutoka kwa Mungu na hiyo inathibitisha kwamba hizo ndizo tunastahili. Hata kama wengine wanalalamika au hawatufurahii, Mimi huamini kila mara kwamba hakuna anayeweza kukubali au kuchukua baraka ambazo Mungu ametupa. Kwa sababu kazi ya Mungu inatekelezwa juu yetu na Ananena nasi ana kwa ana—kwetu sisi, sio kwa wengine—Mungu hufanya chochote Anachotaka kufanya, na ikiwa watu hawaridhiki, huko si kujitakia tu tatizo?

Je, huko si kukaribisha aibu? Ni kwa nini Niseme hili? Ni kwa sababu Nina uzoefu wa kina na hili. Kama tu kazi ambayo Mungu hufanya juu Yangu ambayo ni Mimi tu Niwezaye kuikubali—je, mtu yeyote mwingine anaweza kuifanya? Nina bahati kwamba Mungu amenikabidhi Mimi hili—je, mtu yeyote mwingine angeweza kufanya hilo bila kuchagua kwa busara? Lakini Natarajia kwamba ndugu na dada Zangu wataweza kufahamu moyo Wangu. Sio kushikilia kwa nguvu sifa Zangu mimi kujisifu kwa watu, lakini ni kueleza suala fulani. Niko radhi kumpa Mungu utukufu wote na kumwacha Yeye achunguze kila mojawapo ya mioyo yetu ili mioyo yetu yote itakaswe mbele ya Mungu. Ningependa kutoa ombi moja kwa dhati kabisa: Natarajia kupatwa na Mungu kabisa, kuwa mwanamwali safi anayetolewa kama dhabihu juu ya madhabahu, na hata zaidi kuwa na utii wa mwanakondoo, kujitokeza miongoni mwa wanadamu wote kama mwili mtakatifu wa kiroho. Hii ni ahadi Yangu, kiapo Nilichoanzisha mbele ya Mungu. Niko radhi kuitimiza na kulipa upendo wa Mungu kupitia hii. Je, uko radhi kufanya hili? Naamini kwamba ahadi hii Yangu itawatia moyo ndugu na dada wadogo zaidi, na kuwapa tumaini vijana wadogo zaidi. Nahisi kuwa inaonekana kwamba Mungu huweka sisitizo maalum juu ya vijana. Labda ni upendeleo Wangu mimi, lakini Mimi huhisi kila mara kwamba vijana wana tumaini kuhusu siku zao za baadaye; inaonekana kwamba Mungu hufanya kazi ya ziada katika vijana. Ingawa wanapungukiwa na utambuzi na hekima na wao wote ni wachangamfu kupita kiasi na wakaidi kama ndama aliyezaliwa, Naamini kwamba vijana hawajakosa sifa njema kabisa. Unaweza kuuona umaasumu wa ujana ndani yao na wao ni wepesi kukubali mambo mapya. Ingawa vijana huelekea kwa kiburi, ukali, na uamuzi wa ghafla, mambo haya hayaathiri uwezo wao wa kupokea mwanga mpya. Hii ni kwa sababu vijana kwa jumla huwa hawashikilii sana vitu vya mtindo wa zamani. Hii ndiyo maana Naona matumaini yasiyo na mipaka katika vijana, na uchangamfu wao; ni kutokana na hili ndio maana Nina hisia njema kwao. Ingawa Sina chuki yoyote kwa ndugu na dada wazee, pia sina haja na wao. Mimi Naomba radhi kwa dhati kutoka kwa ndugu na dada wazee. Labda Nilichosema hakifai au ni kisichojali hisia za wengine, lakini Natarajia kwamba nyote mtawia radhi kutojali Kwangu, kwa sababu Mimi ni mdogo sana na Sitilii mkazo sana mwenendo Wangu wa kuzungumza. Hata hivyo, kusema kweli, ndugu na dada wazee, hata hivyo, wana kazi zao wanazopaswa kutenda—wao sio bure kamwe. Hii ni kwa sababu wana uzoefu wa kushughulikia mambo, wako thabiti jinsi wanavyoshughulikia mambo, na hawafanyi makosa mengi sana. Je, huu si uwezo wao? Ningependa sote tuseme mbele ya Mungu: “Ee Mungu! Sote na tuweze kutimiza kazi zetu katika nafasi mbalimbali, na sote tufanye vizuri kabisa tuwezavyo kwa ajili ya mapenzi Yako!” Naamini haya lazima yawe mapenzi ya Mungu!

Kutokana na yale Niliyoona katika uzoefu Wangu, wengi ambao wameupinga mkondo huu, yaani, wengi ambao wamepinga Roho wa Mungu wazi, wamekuwa wazee. Fikira za kidini

ambazo watu hawa wanashikilia ni za nguvu sana na wao hulinganisha mambo ya mtindo wa zamani kwa maneno ya Mungu katika kila hali. Wao kila mara hutumia mambo waliyokubali katika wakati uliopita kwa maneno ya Mungu. Je, wao si wa upuuzi? Inawezekana kuwa watu kama hao wanaweza kufanya kazi waliyopewa na Mungu? Yawezekana kuwa Mungu anaweza kuwatumia watu wa aina hiyo kwa kazi Yake? Roho Mtakatifu ana utaratibu kwa siku yoyote ile ya kazi Yake; ikiwa watu watashikilia mambo ya mtindo wa zamani, siku itakuja ambayo watasukumwa kutoka kwa jukwaa la historia. Katika kila hatua ya kazi Yake, Mungu huwatumia watu wapya kila mara. Ikiwa mtu angewahubiria wengine na mambo yasiyotumika siku hizi, hii haingekuwa tu kuwaangamiza watu? Hii haingekuwa kuchelewesha kazi Yake? Kwa hiyo kazi ya Mungu inaweza kutimizwa lini? Labda kuna wengine ambao wana fikira zingine kuhusu kile ambacho Nimesema sasa. Labda hawataridhishwa. Hata hivyo, Natarajia kwamba huna wasiwasi; mambo mengi kama haya yatafanyika hapo baadaye, na hili linaweza tu kufafanuliwa kupitia kwa ukweli. Huenda hata tukawatembelea watu fulani wa maana, wachungaji fulani wenye hadhi kuu au wafasiri wa Biblia na kuwahubiria mkondo huu. Hapo mwanzo, kwa hakika hawatapinga waziwazi, lakini watachomoa Biblia kushindana na wewe. Watakufanya usimulie Kitabu cha Isaya na Kitabu cha Danieli, na hata watakufanya ueleze Kitabu cha Ufunuo. Na kama hutaweza kuizungumzia, watakukataa, na kukuita Kristo wa uongo, na kusema kwamba unaeneza njia ya upuuzi. Baada ya saa nzima watatoa lawama za uongo dhidi yako mpaka utakosa pumzi. Je, huu si upinzani ulio wazi? Lakini huo ni mwanzo tu. Hawawezi kuzuia hatua inayofuata ya kazi ya Mungu, na kabla ya muda mrefu, Roho Mtakatifu atawalazimisha kuikubali. Huu ni mwelekeo wa jumla; ni kitu ambacho wanadamu hawawezi kukifanya na kitu ambacho watu hawawezi kukiwaza. Naamini kwamba kazi ya Mungu itaenea kote ulimwenguni bila kuzuiwa. Haya ni mapenzi ya Mungu, na hakuna anayeweza kuyazuia. Mungu na atupe nuru na kutufanya tukubali nuru mpya zaidi na sio kuingilia usimamizi wa Mungu katika suala hili. Mungu atuonee huruma ili kwamba sote tuweze kuona kuja kwa siku Yake ya utukufu. Mungu atakapotukuzwa kote katika ulimwengu mzima huo ndio wakati ambao tutapata utukufu pamoja Naye. Inaonekana kwamba huo pia ndio wakati ambao Nitaondoka kwa wale wanaotembea na Mimi. Natarajia kwamba ndugu na dada Zangu watapaza sauti zao pamoja na Yangu kumwomba Mungu: Kazi kuu ya Mungu na ikamilike hivi punde ili tuione siku Yake ya utukufu wakati wa maisha yetu. Bado Natarajia kutimiza mapenzi ya Mungu wakati wa maisha Yangu, na Natarajia kwamba Mungu ataendelea kufanya kazi Yake ndani yetu na kwamba hakutakuwa na vizuizi vyovyote. Hii ndiyo hamu Yangu ya milele. Mungu awe miongoni mwetu kila mara na upendo Wake ujenge daraja kati yetu ili urafiki ulio kati yetu uwe wa thamani zaidi. Natarajia kwamba upendo utasababisha uelewano zaidi kati yetu na kwamba upendo utatufanya tukaribiane kwa upendo, kuondoa pengo lililo kati yetu, na kwamba upendo ulio kati yetu uwe wa kina zaidi, mpana zaidi, na wa kupendeza zaidi. Naamini kwamba haya ni mapenzi ya Mungu. Natarajia

kwamba ndugu na dada Zangu wataweza kuwa karibu sana na Mimi, na kwamba sote tuthamini siku chache tulizo nazo pamoja kwamba zitaweza kuwa kumbukumbu nzuri kwetu.

Kumekuwa na hatua zaidi za kazi ya Mungu katika China bara lakini si zenye utata hata kidogo. Kufikiria juu ya hatua hizo zote, hazikosi sababu—zote zimekamilishwa na Mungu Mwenyewe, na watu wote huchukua nafasi mbalimbali katika kazi Yake. Kila onyesho katika mchezo huu ni la kuchekeka kwa watu, na la ajabu kila mtu ana nafasi ndani yake. Katika kila jaribio, utendaji wa watu huwa wa kweli kwa maisha, na kila mtu amechorwa kwa dhahiri sana na kikamilifu na kalamu ya Mungu. Kila mtu ana mengi yanayofichuliwa katika mwangaza wa siku. Sisemi kwamba Mungu anawadhihaki watu kupitia kwa kazi Yake; hakungekuwa na maana katika hilo. Kazi yote ya Mungu ina kusudi lake; bila shaka Hafanyi chochote kisichokuwa na umuhimu au thamani. Mambo yote Ayafanyayo ni ya kuwakamilisha na kuwapata wanadamu. Ni kutoka tu kwa hayo ndio Nimeona kweli kwamba moyo wa Mungu wote ni kwa wema wa mwanadamu. Ingawa unaweza kuitwa mchezo wa kuigiza, inaweza pia kusemwa kwamba mchezo huu wa kuigiza ni mfano wa maisha ya kweli, lakini kwa mwendeshaaji mkuu wa tamthiliya, Mungu, watu wote wanatakiwa kushirikiana ili kuikamilisha kazi hii. Lakini kutoka upande mwingine, Mungu huwapata watu kupitia hili na kuwafanya watu wampende Yeye zaidi. Je, haya si mapenzi Yake? Kwa hiyo Natarajia kwamba hakuna aliye na matatizo. Je, hujui lolote kuhusu mapenzi ya Mungu? Nimesema mengi sana—Natarajia kwamba ndugu na dada Zangu wote wanaweza kufahamu na sio kutofahamu moyo Wangu. Naamini kwamba Mungu atawapata kikamilifu. Kila mtu hutembea njia tofauti. Natarajia kwamba njia iliyo chini ya miguu yenu ni ile ambayo imefunguliwa na Mungu, na kwamba nyote mtaomba na kusema: “Ee Mungu! Nipate mimi ili roho yangu ikurudie Wewe.” Je, uko tayari kutafuta uongozi wa Mungu ndani ya kina cha roho yako?

Njia ... (5)

Hapo zamani, hakuna aliyemjua Roho Mtakatifu, sembuse kujua njia iliyotembelewa na Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo sababu watu daima wamejipumbaza mbele za Mungu. Ni sawa kusema kwamba karibu kila mtu anayemwamini Mungu hamjui Roho, na kwamba imani yao imekanganyika na kutatizika. Ni dhahiri kwamba watu hawamwelewi Mungu; na ingawa kwa vinywa vyao wanaweza kusema kwamba wanamwamini, kimsingi, kwa kutegemeza tabia yao, wanajiamini, sio Mungu. Katika yale ambayo kwa kweli Nimeyapitia mwenyewe, Nimeona kwamba Mungu anamshuhudia Mungu mwenye mwili, na kutoka nje inaonekana kuwa watu wamelazimishwa kukiri ushuhuda wa Mungu, kwa kiwango kidogo sana inaweza kusemekana kuwa wanaamini kwamba Roho wa Mungu hana makosa hata kidogo. Hata hivyo, Nasema kwamba kile ambacho watu wanaamini si mtu huyu, sembuse Roho wa Mungu, ila ni hisia zao

wenyewe. Je, hawajiamini tu kwa kufanya hilo? Nisemacho ni ukweli. Mimi siwabandiki watu majina, lakini kuna jambo moja ambalo lazima Nieleze wazi: Ili watu waletwe hadi leo, iwe wameelewa ama wamekanganyikiwa, yote ni kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Silo jambo ambalo wanadamu wanaweza kulidhibiti. Huu ni mfano wa kile Nilichotaja awali kuhusu Roho Mtakatifu kulazimisha imani ya watu; hii ndiyo njia ambayo Roho Mtakatifu hufanya kazi, na ndiyo njia aliyoichukua Roho Mtakatifu. Bila kujali yule ambaye watu wanamwamini kimsingi, Roho Mtakatifu huwapa watu hisia fulani kwa lazima, Akiwafanya wamwamini Mungu mioyoni mwao. Je, hivyo sivyo unavyoamini? Je, huhisi kwamba imani yako katika Mungu ni jambo la ajabu? Je, hudhani kuwa ni jambo lisilo la kawaida kwamba huwezi kuepuka mkondo huu? Je, hujatia juhudi yoyote katika kulifikiria hili? Je, huu si muujiza na ishara kubwa zaidi kati ya yote? Hata kama umekuwa na hamu kubwa ya kuhepa mara nyingi, daima kuna nishati uhai yenye nguvu inayokuvutia na kukufanya usite kuondoka. Na kila wakati unapojipata katika hali kama hizi, unaanza kulia na kutoa machozi kila wakati, usijue cha kufanya baada ya hapo. Wengine wenu hujaribu kuondoka, lakini unapojaribu kuenda, unahisi uchungu sana, unahisi kana kwamba zimwi fulani wa dunia ameichukua nafsi yako kutoka kwako, akiuacha moyo wako bila utulivu na bila amani. Baada ya hapo, huna budi ila kujikaza na kumrudia Mungu. ... Je, hujapitia hili? Sina shaka kwamba ndugu wadogo, wanaoweza kuifungua mioyo yao watasema: “Ndiyo! Nimepitia hili mara nyingi sana, naaibika kuliwaza!” Katika maisha Yangu mwenyewe ya kila siku, daima Nina furaha kuwachukulia ndugu Zangu kama wandani Wangu, kwa sababu hawana hatia hata kidogo—wao hawana madoa na ni wazuri sana. Wao ni kama marafiki Wangu. Hiyo ndiyo maana daima Natafuta nafasi ya kuwaleta pamoja wandani Wangu wote ili kuzungumzia mawazo yetu na mipango yetu. Mapenzi ya Mungu na yatimike ndani yetu ili sote tuwe ndugu wa karibu, bila vikwazo ama umbali kati yetu. Na sote tumwombe Mungu: “Ee Mungu! Ikiwa ni mapenzi Yako, tunakusihi Utupe mazingira yanayofaa, ili tuweze kutimiza matakwa Yako mioyoni mwetu. Utuhurumie sisi vijana tusio na mantiki, na uturuhusu tutumie nguvu iliyo ndani ya mioyo yetu!” Naamini kwamba haya ni mapenzi ya Mungu, kwani zamani za kale Nilimwomba Mungu na kusema: “Baba! Duniani, tunakulilia bila kikomo, tukitaka mapenzi Yako yaweze kufanyika duniani hivi karibuni. Ningependa kutafuta mapenzi Yako. Na Ufanye utakacho kufanya na Ukamilishe agizo Lako ndani Yangu kwa haraka sana. Hata Niko tayari kwa Wewe kufungua njia mpya miongoni mwetu, ikiwa hili litamaanisha kwamba mapenzi Yako yatatimika karibuni! Naomba tu kwamba kazi Yako iweze kukamilika karibuni, na Naamini kwamba hakuna sheria zinazoweza kuizuia!” Kazi ya Mungu iko hivi leo; je, huoni njia ambayo Roho Mtakatifu anaitembelea? Kila wakati Ninapokutana na ndugu wenye umri mkubwa, Nahisi kukandamizwa sana. Ninapokutana nao, Naona kwamba wanadhihirisha jamii; fikira zao za kidini, uzoefu wao wa kuyashughulikia mambo, namna yao ya kuzungumza, maneno wanayoyatumia, na kadhalika—wote wanaudhi. Wanakisiwa kuwa na “hekima.” Daima

huwa Najitenga nao kabisa, kwa sababu Mimi binafsi sijajihami kwa falsafa za kuishi duniani. Kila wakati Nikutanapo na watu hawa, wananiacha Nikiwa nimechoka, kichwa Changu kikijawa jasho; wakati mwingine Nahisi kukandamizwa sana kiasi kwamba Naishiwa na pumzi. Hivyo katika wakati huu wa hatari, Mungu ananipa suluhisho zuri. Huenda ni kuelewa Kwangu vibaya tu. Najali tu kuhusu linalomfaidi Mungu; lililo muhimu zaidi ni kufanya mapenzi ya Mungu. Najitenga kabisa na watu hawa, lakini ikiwa Mungu ananihitaji kukutana nao, bado Natii. Si kwamba wao wanasinya, ila kuwa “hekima,” fikira na falsafa zao za kuishi duniani zinachukiza sana. Niko hapo ili kukamilisha agizo la Mungu, sio kujifunza jinsi wanavyofanya mambo. Nakumbuka jinsi Mungu alivyowahi kuniambia, “Duniani, tafuta tu kufanya mapenzi ya Baba Yako na Ukamilishe agizo Lake. Hakuna jingine linalokuhusu.” Napata amani kidogo Ninapolifikiria hili. Hiyo ni kwa sababu masuala ya binadamu daima hunitatiza sana; Siwezi kuyaelewa, na kamwe Sijui la kufanya. Kwa hivyo nyakati nyingi Nimehangaishwa na hili na Nimewachukia wanadamu; mbona watu lazima wawe wagumu sana? Mbona hawawezi kuwa wa kawaida? Mbona mtu ajaribu kuwa mjanja sana? Nikutanapo na watu, wakati mwingi kunategemezwa kwa agizo la Mungu Kwangu. Kunaweza kuwa na nyakati chache ambapo hali haikuwa hivyo, lakini ni nani ajuaye kilichofichika katika vina vya moyo Wangu?

Mara nyingi Nimewashauri ndugu walio nami kwamba wanapaswa kumwamini Mungu kwa dhati, kwamba hawapaswi kujali masilahi yao wenyewe, ila wayazingatie mapenzi ya Mungu. Mara nyingi Nimelia kwa uchungu mbele za Mungu: Mbona watu hawayazingatii mapenzi ya Mungu? Hakika kazi ya Mungu haiwezi tu kutoweka isionekane tena bila sababu? Wala Sijui mbona—hili limekaribia kuwa fumbo akilini Mwangu—mbona watu hawaitambui njia iliyotembelewa na Roho Mtakatifu kamwe, lakini wanaendelea kuyashikilia mahusiano yasiyo ya kawaida waliyo nayo na wengine? Nachafuka moyo Niwaonapo watu wakiwa namna hii. Badala ya kuitumainia njia ya Roho Mtakatifu, wanalenga matendo ya mwanadamu. Je, Mungu anaweza kuridhishwa na hili? Mara nyingi huwa Nasikitishwa na hili. Limekaribia kuwa mzigo Wangu—na linamsumbua Roho Mtakatifu pia. Je, huhisi lawama yoyote moyoni mwako? Naomba Mungu afungue macho ya roho yako. Mara nyingi Mimi, Ninayewaongoza watu kuingia katika kazi ya Mungu, Nimeomba mbele za Mungu: “Ee Baba! Ningependa mapenzi Yako yawe kiini, Ningependa kutafuta mapenzi Yako, Ningependa kwamba Niwe mwaminifu kwa agizo Lako, ili Uweze kulipata kundi hili la watu. Nakuomba Utupeleke katika nchi ya uhuru, ili tuweze kukugusa kwa roho Zetu, na Naomba Uzindue hisia za kiroho zilizo mioyoni mwetu!” Ningependa kwamba mapenzi ya Mungu yatimike, na kwa hiyo Naomba bila kikomo kwamba Roho Wake aendeleo kutupa nuru, kwamba tuweze kuitembea njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu—kwani njia Niitembeayo ni njia ya Roho Mtakatifu. Na ni nani mwingine anayeweza kuitembea njia hii badala Yangu? Hili ndilo linaloufanya mzigo Wangu kuwa mzito

hata zaidi. Nahisi kana kwamba Ninakaribia kuanguka, lakini Nina imani kwamba Mungu hawezi kamwe kuchelewesha kazi Yake. Huenda tutatengana tu mara agizo Lake litakapokamilishwa. Kwa hiyo labda ni kwa sababu ya matokeo ya Roho wa Mungu ndiyo daima Nimehisi tofauti. Ni kana kwamba kuna kazi ambayo Mungu anataka kufanya, lakini bado Siwezi kuelewa ni ipi. Lakini Naamini kwamba hakuna mtu duniani aliye bora kuliko wandani Wangu, na Naamini kwamba wataniombea mbele za Mungu, na kwa sababu ya hilo Nina shukrani isiyo na kipimo. Ningewataka ndugu Zangu waseme nami: “Ee Mungu! Na mapenzi Yako yadhihirike kikamilifu ndani yetu sisi, watu wa enzi ya mwisho, ili tuweze kubarikiwa na uzima wa roho, na kutazama matendo ya Roho wa Mungu, na kuutazama uso Wake wa kweli!” Punde tunapofikia hatua hii kweli tutakuwa tukiishi chini ya mwongozo wa Roho, na hapo tu ndipo tutaweza kuutazama uso wa kweli wa Mungu. Yaani, watu wataweza kuelewa maana halisi ya ukweli wote, sio kufahamu ama kuelewa kulingana na fikira za binadamu, ila kulingana na nuru ya mapenzi ya Roho wa Mungu. Hii yote ni kazi ya Mungu Mwenyewe, hakuna lolote litokalo katika mawazo ya binadamu ndani yake; ni mpango Wake wa kazi kwa ajili ya matendo Anayotaka kudhihirisha duniani, na ndiyo sehemu ya mwisho ya kazi Yake duniani. Je, ungependa kujiunga na kazi hii? Je, unataka kujihusisha nayo? Je, unatamani kukamilishwa na Roho Mtakatifu na kushiriki katika uzima wa roho?

Kilicho muhimu leo ni kuingia kwa kina zaidi kutoka kwa msingi wetu wa asili. Lazima tuingie kwa kina zaidi katika ukweli, maono, na uzima—lakini kwanza lazima Niwakumbushe ndugu kwamba ili kuingia hatua hii ya kazi, lazima uachane na fikira zako za awali. Yaani, lazima ubadili jinsi unavyoishi, ufanye mipango mipya, ujirekebishe na kuanza upya. Ikiwa bado unashikilia kile kilichokuwa cha thamani kwako zamani, Roho Mtakatifu hataweza kufanya kazi ndani yako, na Atakimu maisha yako kwa shida. Wale ambao hawafuatili, ama kuingia, ama kupanga wataachwa kabisa na Roho Mtakatifu—na kwa hivyo wanasemekana kwamba wametelekezwa na enzi. Natumai kwamba ndugu wote wanaweza kuuelewa moyo Wangu, na Natumai kwamba “wanachama wapya” watasimama kushirikiana na Mungu na wakamilishe kazi hii pamoja. Naamini kwamba Mungu atatubariki. Naamini pia kwamba Mungu atanipa wandani wengi zaidi, ili Niweze kutembea kwa kila pembe ya dunia, na kuweza kuwa na upendo mkubwa zaidi kati yetu. Aidha, Naamini kwamba Mungu ataueneza ufalme Wake kwa sababu ya juhudi zetu; Ningependa kwamba hizi juhudi zetu zifike viwango ambavyo havijawahi kufikiwa awali, zikimruhusu Mungu awapate vijana zaidi. Ningependa tutumie muda zaidi tukiombea hili, Ningependa tuombe bila kukoma, ili tuishi maisha yetu yote mbele za Mungu, na tuwe karibu iwezekanavyo na Mungu. Naomba kusiwe na chochote kati yetu tena, na naomba sote tukule kiapo hiki mbele za Mungu: Kufanya kazi pamoja kwa bidii! Kuwa waaminifu hadi mwisho kabisa! Kutowahi kutengana, na kuwa pamoja daima! Natumai kwamba ndugu wote watoe ahadi

hii mbele za Mungu, ili mioyo yetu isibadilike kamwe, na azma yetu isiyumbayumbe kamwe! Kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, Nasema tena: Tufanye kazi kwa bidii! Tujitahidi kwa uwezo wetu wote! Hakika Mungu atatubariki!

Njia ... (6)

Tumeletwa hadi siku ya leo kwa sababu ya kazi ya Mungu, na kwa hiyo sisi ndio waliosalia katika mpango wa Mungu wa usimamizi. Kwamba tumebaki leo ni kuinuliwa pakubwa na Mungu, kwani kulingana na mpango wa Mungu, nchi ya joka kubwa jekundu inapaswa kuangamizwa. Lakini Nadhani kwamba huenda Ameanzisha mpango mwingine, ama Anataka kutekeleza sehemu nyingine ya kazi Yake, kwa hiyo hata leo, Siwezi kueleza hili vizuri—ni kama fumbo lisiloweza kufumbulika. Lakini kwa jumla, hili kundi letu limeamuliwa kabla na Mungu, na Ninaendelea kuamini kwamba Mungu ana kazi nyingine ndani yetu. Nasi sote tusihi Mbingu hivi: “Mapenzi Yako yatimie, na Utuonekanie tena na Usijifiche ili tuweze kuona utukufu Wako na uso Wako vizuri zaidi.” Kila wakati Nahisi kwamba njia ambayo Mungu hutuelekezea siyo nyoofu, ila ni njia iliyopinda ambayo imejaa mashimo; aidha, Mungu husema kwamba kadiri njia ilivyo yenye miamba zaidi, ndivyo inavyoweza kufichua mioyo yetu ya upendo zaidi. Lakini hakuna kati yetu anayeweza kuifungua njia kama hii. Katika yale Niliyoyapitia, nimezitembea njia nyingi ngumu zenye miamba na Nimevumilia mateso makubwa; nyakati nyingine Nimekuwa na huzuni nyingi sana kiasi kwamba Nimetaka kulia, lakini Nimeitembea njia hii hadi wa leo. Naamini kwamba hii ndiyo njia inayoongozwa na Mungu, kwa hiyo Navumilia maumivu makali ya dhiki yote na Ninaendelea kusonga mbele. Kwani hili ndilo ambalo limeamuliwa na Mungu, kwa hiyo ni yupi anayeweza kuliepuka? Sitaki kupata baraka zozote; Ninachotaka tu ni kwamba Niweze kuitembea njia Ninayopaswa kuitembea kulingana na mapenzi ya Mungu. Sitaki kuwaiga wengine, Nikiitembea njia wanayoitembea; Nitakacho tu ni kwamba Niweze kutimiza kujitoa Kwangu katika kuitembea njia Niliyochaguliwa hadi mwisho. Siwataki wengine wanasaidie; kusema ukweli, Siwezi kumsaidia mwingine yeyote pia. Inaonekana kwamba Mimi ni mwepesi sana wa kuhisi kuhusiana na jambo hili. Sijui wanachofikiria watu wengine. Hii ni kwa sababu daima Nineamini kwamba kiasi ambacho mtu lazima ateseke na umbali ambao lazima autembe kwenye kinjia yake yameamuliwa na Mungu, na kwamba hakuna yeyote anayeweza kumsaidia mwingine kweli. Ndugu zetu wengine wenye ari wanaweza kusema kwamba Sina upendo, lakini hiki ndicho Ninachoamini tu. Watu wanazitembea njia zao wakitegemea mwongozo wa Mungu, na Ninaamini kwamba ndugu Zangu wengi watauelewa moyo Wangu. Natumai pia kwamba Mungu atatupa nuru kubwa zaidi katika kipengele hiki, ili upendo wetu uweze kuwa safi zaidi na urafiki wetu uwe wa thamani zaidi. Naomba tusikanganywe kuhusu mada hii, ila tupate ufahamu mkubwa zaidi tu, ili mahusiano baina yetu yaweze kujengwa juu ya msingi wa uongozi wa

Mungu.

Mungu amefanya kazi katika bara China kwa miaka kadhaa, na Amelipa gharama kubwa kwa wanadamu wote ili atufikishe tulipo leo. Nadhani kwamba ili kuwaongoza watu wote kwenye njia sahihi, kazi hii lazia ianze kwenye udhaifu wa kila mtu; hapo tu ndipo wanaweza kukishinda kikwazo cha kwanza na kuendelea kusonga mbele. Si hilo ni bora? Taifa la China, likiwa limepotoshwa kwa miaka mingi, limesalia hadi leo, kila aina ya “virusi” vikizidi bila kikomo, vikienea kila mahali kama pigo; inatosha tu kuangalia mahusiano ya watu ili kuona jinsi “vijidudu” vingi vimejificha ndani ya watu. Ni vigumu sana kwa Mungu kukuza kazi Yake katika eneo lililobanwa sana na kujawa virusi. Hulka za watu, tabia, jinsi wanavyofanya mambo, kila kitu wanachoonyesha katika maisha yao na mahusiano baina yao—yote yameharibika, kufikia kiwango ambapo ufahamu na utamaduni wa kibinadamu yote yamehukumiwa kufa na Mungu. Sembuse uzoefu mbalimbali waliojifunza kutoka kwa familia na jamii zao—hawa wote wamepatikana kuwa na hatia machoni pa Mungu. Hii ni kwa sababu wale wanaoishi katika nchi hii wamevila virusi vingi sana. Ni kama mambo hayajabadilika kwao, hawajali hili. Kwa hiyo, kadiri watu walivyo wapotovu mahali fulani, ndivyo mahusiano baina yao yanavyozidi kuwa yasiyo ya kawaida. Mahusiano ya watu yamejaa njama, wanakuliana njama na kuuana kana kwamba wako katika ngome ya mapepo ambapo watu hulana. Katika mahali palipojaa hofu kama hapa, ambapo mazimwi wamejaa, ni vigumu sana kutekeleza kazi ya Mungu. Namwomba Mungu bila kukoma inaponibidi Nikutane na watu, kwani Ninahofia kukutana nao, na kuogopa sana kwamba Nitaikosea “heshima” yao na tabia Yangu. Moyoni Mwangu, daima Naogopa kwamba roho hizi chafu zitatenda bila kujali, kwa hiyo daima Namwomba Mungu anilinde. Kila namna ya mahusiano yasiyo ya kawaida yako dhahiri miongoni mwetu, na Nionapo haya yote, kuna chuki moyoni Mwangu, kwani miongoni mwao, watu daima wanajihusisha katika “biashara” ya mwanadamu, na kwamwe hawamfikirii Mungu hata kidogo. Nadharau tabia yao kabisa. Kinachoweza kuonekana ndani ya watu wa bara China ni tabia potovu za kishetani pekee, kwa hivyo katika kazi ya Mungu ndani ya hawa watu, ni vigumu sana kupata chochote cha thamani ndani yao; kazi yote inafanywa na Roho Mtakatifu, na ni kwamba tu Roho Mtakatifu anawagusa watu zaidi, na kufanya kazi ndani yao. Ni vigumu sana kuwatumia watu hawa; yaani, kazi ya Roho Mtakatifu kuwagusa watu pamoja na ushirika wa watu hayawezi kufanyika. Roho Mtakatifu anafanya tu kazi kwa bidii ili kuwagusa watu, lakini hata hivyo, watu wanabakia wenye ganzi na wasiohisi na hawajui anachofanya Mungu hata kidogo. Kwa hiyo, kazi ya Mungu huko bara China inalingana na kazi Yake ya kuumba mbingu na dunia. Anawafanya watu wote wazaliwe tena, na kubadili kila kitu kuwahusu, kwani hakuna kilicho cha thamani ndani yao. Ni jambo la kuhuzunisha sana. Mara nyingi huwa Ninawaombea watu hawa kwa huzuni: “Mungu, nguvu Yako kuu na ifichuliwe ndani ya watu hawa, ili Roho Wako aweze

kuwaguza sana, na ili watu hawa wenye ganzi na wajinga ambao wanateseka waweze kuzinduka, kamwe wasiwe katika hali ya usingizi mzito, na waone siku ya utukufu Wako.” Na sote tuombe mbele za Mungu na kusema: Ee Mungu! Na Utuhurumie na kututunza tena ili mioyo yetu iweze kukugeukia kikamilifu, na ili tuweze kuikimbia nchi hii chafu, tusimame na kukamilisha kile Ulichotuaminia nacho. Natumai kwamba Mungu ataweza kutugusa tena ili tuweze kupata nuru Yake, na Natumai kwamba Anaweza kutuhurumia ili mioyo yetu iweze kumrudia polepole na Aweze kutupata. Hili ndilo tamanio letu sote.

Njia tuitembeayo imeamuliwa kikamilifu na Mungu. Kwa ufupi, Naamini kwamba hakika Nitaitembea njia hii hadi mwisho kabisa, kwani Mungu daima ananipa tabasamu, na ni kana kwamba daima Naongozwa na mkono Wake. Hivyo moyo Wangu hauchafuliwi na chochote kingine, na hivyo daima Naizingatia kazi ya Mungu. Natekeleza yote ambayo Mungu ananiagiza kwa uwezo Wangu wote na kwa moyo, na kamwe Siingilii kazi ambazo Sijatengewa, wala Sijihusishi na yule anayezifanya—kwa kuwa Naamini kwamba kila mtu lazima aitembee njia yake mwenyewe, na asiingilie ya wengine. Nayaona mambo hivi. Huenda hii ni kwa sababu ya hulka Yangu mwenyewe, lakini Ninatumai kwamba ndugu Zangu wanaelewa na kunisamehe kwa sababu kamwe Sithubutu kuzipinga amri za Baba Yangu. Sithubutu kuyaasi mapenzi ya Mbinguni. Je, Umesahau kwamba “mapenzi ya Mbinguni hayawezi kuasiwa”? Watu wengine wanaweza kunifikiria kuwa mwenye kujifikiria tu, lakini Naamini kwamba Nimekuja hasa ili kutekeleza sehemu moja ya kazi ya Mungu ya usimamizi. Sijaja ili kujihusisha na mahusiano baina ya watu; kamwe Sitajifunza jinsi ya kuelewana na wengine. Hata hivyo, katika agizo la Mungu, Nina mwongozo wa Mungu, na Nina imani na uthabiti wa kutimiza kazi hii. Labda “Najifikiria mwenyewe tu” sana, lakini Natumai kwamba kila mtu atachukua jukumu la kujaribu kuhisi upendo wa Mungu ulio wa haki na usio na ubinafsi, na ajaribu kushirikiana na Mungu. Usisubiri kuja kwa mara ya pili kwa uadhama wa Mungu; hilo halimfaidi yeyote. Daima Nafikiri kwamba kile tunachopaswa kuzingatia ni hiki: “Lazima tufanye kila kiwezekanacho kutenda kile tupaswacho ili kumridhisha Mungu. Agizo la Mungu kwa kila mmoja wetu ni tofauti; tunapaswa kulitimizaje?” Lazima utambue njia uitembeayo ni ipi hasa—ni muhimu kwamba uelewe hili. Kwa kuwa nyote mngependa kumridhisha Mungu, mbona msijikabidhi Kwake? Mara ya kwanza Nilipomwomba Mungu, Nilimpa moyo Wangu wote. Watu walio karibu nami—wazazi, ndugu na wafanyakazi wenza—wote walipuuzwa na kile Nilichokuwa nimeazimia, ilikuwa kana kwamba Kwangu hawakuweko hata kidogo. Kwani kila wakati Nilimfikiria Mungu, ama maneno ya Mungu, ama hekima Yake; mambo haya yalikuwa moyoni mwangu daima, na yalishikilia sehemu yenye thamani zaidi moyoni Mwangu. Kwa hiyo, kwa watu waliojaa falsafa za kuishi, Mimi ni mtu katili na asiyehisi. Mioyo yao inaumizwa na jinsi Ninavyojiheshimu, na jinsi Nifanyavyo mambo, na kila kitendo Changu. Wananiangalia kwa namna ya ajabu, kana

kwamba mtu Niliye ni fumbo lisiloweza kufumbulika. Akilini mwao, wananipima kwa siri, wakipima kwa mizani ya mtu niliye wasijue Nitakachofanya baada ya hapo. Chochote wafanyacho kinawezaje kunizuia? Pengine wana wivu, ama wametishika, ama wananidhihaki; bila kujali, Naomba mbele za Mungu kila wakati kana kwamba Nina njaa na kiu kubwa, kana kwamba ni Mimi na Yeye tu katika dunia moja, na hakuna mtu mwingine yeyote. Nguvu za dunia ya nje hujazana zikinikaribia kila wakati—lakini pia hisia ya kuguswa na Mungu inajaa ndani Yangu. Nikiwa nimekabiliwa na mtanziko huu, Niliinama mbele za Mungu: “Ee Mungu! Ninawezaje kutotaka mapenzi Yako? Unanitazama kama aliye mwenye heshima, kama dhahabu iliyofuliwa, lakini Siwezi kuepuka nguvu za giza. Naweza kuteseka kwa ajili Yako maisha Yangu yote, Naweza kufanya kazi Yako iwe kazi ya maisha Yangu, na Nakuomba unipe mahali panapofaa pa pumziko ili Nijitolee Kwako. Ee Mungu! Ningependa kujitolea Kwako. Unajua udhaifu wa mwanadamu vizuri, kwa hiyo mbona Unajificha kutoka Kwangu?” Papo hapo, ilikuwa kana kwamba Nilikuwa yungiyungi la milimani wasilolijua watu, harufu yake nzuri ikisisimuliwa na upepo mwanana. Hata hivyo, Mbingu ililia, na moyo Wangu uliendelea kulia; Nilihisi kana kwamba kulikuwa na uchungu mkubwa hata zaidi moyoni Mwangu. Nguvu zote na kuzungukwa kwa mwanadamu—yalikuwa kama radi katika siku shwari. Ni nani angeweza kuuelewa moyo Wangu? Na kwa hiyo Nilikuja mbele za Mungu tena na kusema, “Ee Mungu! Hakuna namna ya kutekeleza kazi Yako katika nchi hii yenye uchafu? Mbona wengine hawawezi kuzingatia moyo Wako kwa mazingira ya kustarehesha, ya fadhila ambayo hayana mateso? Nataka kutandaza mabawa Yangu, lakini kwa nini ni vigumu sana kuondoka kwa kupuruka? Je, huliidhinishi?” Nililia kwa sababu ya hili kwa siku kadhaa, lakini daima Niliamini kwamba Mungu angeuletea moyo Wangu wenye huzuni faraja. Hakuna mtu ambaye amewahi kuelewa wasiwasi Wangu. Huenda ni utambuzi wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu—Mimi daima Nimekuwa na shauku ya kazi Yake ndani Yangu, na Sijapata hata muda wa kupumua. Hadi leo, bado Naomba na kusema, “Ee Mungu! Ikiwa ni mapenzi Yako, Naomba Uniongoze kutekeleza kazi Yako hata kubwa zaidi ili iweze kuenea ulimwenguni kote, na ili iweze kufunuliwa kwa kila taifa na dhehebu, ili moyo Wangu uwe na amani kidogo, na ili Niweze kuishi mahali pa pumziko kwa ajili Yako, na Niweze kukufanyia kazi bila kukatizwa, na Niweze kukutumikia, moyo Wangu ukiwa na amani, kwa maisha Yangu yote.” Hili ndilo tamanio la moyo Wangu. Huenda ndugu watasema kwamba Mimi ni mwenye majivuno na Anayejiipenda; nami pia Nakiri hili, kwani ni ukweli—vijana ni wenye majivuno kabisa. Kwa hiyo Nasema mambo kama yalivyo, bila kupinga ukweli. Huenda ukaona hulka zote za kijana ndani Yangu, lakini pia unaweza kuona Niliko tofauti na vijana wengine. Utulivu na ukimya Wangu. Siyazungumzii haya kwa undani; Naamini kwamba Mungu ananijua vyema kuliko Nijijuavyo. Haya ni maneno yatokayo moyoni Mwangu, na Natumai kwamba ndugu hawatachukizwa. Tuyazungumzie maneno yaliyo miyoni mwetu, tuangalie ni kipi ambacho kila mmoja wetu

anakifuatilia, tulinganishe mioyo yetu ya upendo kwa Mungu, tuyasikilize maneno tunayomnong’onezea Mungu, tuziimbe nyimbo nzuri zaidi mioyoni mwetu, na tudhihirishe fahari iliyo mioyoni mwetu, ili maisha yetu yaweze kuwa mazuri zaidi. Tuyasahau yaliyopita na tuyaganje yajayo. Mungu atatufungulia njia!

Njia ... (7)

Katika yale tunayoyapitia kwa vitendo, tunaona kwamba kuna nyakati nyingi ambapo Mungu ametufungulia njia yeye binafsi, ili njia tunayoitembea iweze kuwa thabiti zaidi na halisi zaidi. Kwani hii ndiyo njia ambayo Mungu ametufungulia tangu zamani za kale, na ambayo kizazi chetu kimepitishwa baada ya miaka mingi sana. Kwa hiyo tumeishika njia ya wale waliotutangulia, ambao hawakuitembea mpaka mwisho. Tumechaguliwa na Mungu kutembea hatua yake ya mwisho. Na kwa hiyo, tuliandaliwa njia hii hasa na Mungu, na bila kujali iwapo tumebarikiwa ama kukabiliwa na msiba, hakuna mtu mwingine anayeweza kuitembea njia hii. Ningependa kuongeza ufahamu Wangu mwenyewe kwa jambo hili: Usifikirie kujaribu kutorokea kwingine, ama kujaribu kupata njia nyingine, na usitamani hadhi, ama kujaribu kuanzisha ufalme wako mwenyewe—hizi zote ni njozi. Unaweza kuwa na fikira fulani za awali kuhusu maneno Yangu, na hali ikiwa hivyo, Ningependekeza kwamba uache kukanganyika sana. Itakuwa bora ukilifikiria hili zaidi; usijaribu kuwa mjanja, na usiyachanganye mabaya na mema. Utajuta hilo mara tu mpango wa Mungu unapotimia. Ninachosema ni kuwa, ufalme wa Mungu utakapofika, mataifa yote ya dunia yataavunjwa vipande vipande. Wakati huo utaona kwamba mipango yako mwenyewe pia imeharibika, na kwamba wale ambao wanaadibiwa wataangamizwa, na Mungu atadhihirisha tabia Yake kikamilifu kupitia hili. Nadhani kwamba kwa kuwa mambo haya ni dhahiri sana Kwangu, napaswa kukuambia kuyahusu, ili usinilaumu baadaye. Kwamba tumeweza kuitembea njia hii hadi leo kuliamuliwa na Mungu, kwa hiyo usifikiri kwamba wewe ni mtu wa kipekee, wala kuwa huna bahati—hakuna anayeruhusiwa kutoa maoni kuhusu kazi ya sasa ya Mungu asije akavunjwa vipande vipande. Nimetiwa nuru na kazi ya Mungu: Hali iweje, Mungu atalikamilisha kundi hili la watu, kazi Yake haitawahi kubadilika tena, na Atalichukua kundi hili la watu hadi mwisho wa njia, na kukamilisha kazi Yake duniani. Sote tunapaswa kuelewa hili. Watu wengi wanapenda “kutazamia mbele,” na tamaa zao haziishi. Hakuna yeyote kati yao anayeelewa mapenzi ya Mungu ya leo yaliyo dharura, na kwa hiyo wote wanafikiri kuhusu kutoroka. Wao ni kama farasi waliotoroka wanaotaka tu kuzurura mwituni; ni wachache wanaotaka kuishi katika nchi nzuri ya Kanaani ili kutafuta njia ya maisha ya binadamu. Watu wasipofurahia nchi iliyojaa maziwa na asali baada ya kuiingia, ni nini zaidi wanachotaka basi? Kusema ukweli, kuna mwitu tu nje ya nchi nzuri ya Kanaani. Hata baada ya watu kuingia mahali pa pumziko, hawawezi kufanya wajibu wao; je, si wao ni makahaba tu? Ukipoteza nafasi ya kukamilishwa na Mungu hapa, utajuta milele, majuto

yako hayatakuwa na kikomo. Utakuwa kama Musa aliyeiona nchi ya Kanaani lakini hakuweza kuifurahia, makonde yake yakiwa yamekazwa sana, na kifo chake kujaa majuto—hudhani hili kuwa jambo la haya? Hulioni kuwa jambo la aibu, la kukejeliwa na wengine? Je, uko tayari kufedheheshwa na wengine? Je, hutaki kuwa na maisha mazuri? Je, hutaki kuwa mtu mwenye heshima na mwadilifu anayekamilishwa na Mungu? Je, kweli huna hamu ya kufanikisha chochote? Huko tayari kuzichukua zile njia nyingine; je, pia hutaki kuichukua njia ambayo Mungu amekuamulia? Je, unathubutu kuyapinga mapenzi ya Mbinguni? Bila kujali jinsi “ustadi” wako ulivyo wa juu, kweli unaweza kuikosea Mbingu? Naamini kwamba ni heri tujaribu kujijua vyema. Neno moja kutoka kwa Mungu linaweza kubadili mbingu na dunia, sembuse mtu mdogo dhaifu machoni pa Mungu?

Katika yale niliyoyapitia Mimi mwenyewe, Nimeona kwamba kadiri unavyozidi kumpinga Mungu, ndivyo Mungu atakavyoonyesha tabia Yake adhimu zaidi, na ndivyo Atakavyokuadibu vikali zaidi; kadiri unavyozidi kumtii, ndivyo Atakavyokupenda na kukulinda zaidi. Tabia ya Mungu ni kama chombo cha adhabu: Ukitii utakuwa salama salimini; wakati hutii—wakati unajaribu kujiringa kila wakati, na kucheza shere kila wakati—tabia ya Mungu inabadilika mara moja. Yeye ni kama jua katika siku yenye mawingu mengi, Atajificha kutoka kwako na kukuonyesha hasira Yake. Tabia Yake pia ni kama hali ya hewa ya mwezi wa Juni, ambapo anga ni shwari kwa mwendo mrefu na maji yako matulivu, mpaka wakati ambapo mkondo unaenda kwa kasi ghafla, na maji yanaanza kuwa na msukosuko wa mawimbi. Je, unaweza kuthubutu kutojali kiasi hiki ukiwa umekabiliwa na tabia kama hii ya Mungu? Katika uzoefu wenu, wengi wenu ndugu mmeona kwamba Roho Mtakatifu anapofanya kazi mchana, mnajawa na imani—lakini bila kutarajia, Roho wa Mungu anakutelekeza ghafla, na unasumbuka sana kiasi kwamba huwezi kulala usiku, ukitafuta huku na kule mahali ambapo Roho Wake ametoweka. Bila kujali unachofanya, huwezi kupata alikoenda Roho Wake—lakini ghafla, Anakuonekana tena, na unafurahi sana kama wakati Petro kwa ghafla alimtazama Bwana wake Yesu mara nyingine, unafurahi sana kiasi kwamba karibu ulie. Kweli umesahau hili baada ya kulipitia mara nyingi sana? Bwana Yesu Kristo, aliyepata mwili, aliyetundikwa msalabani, na kisha akafufuka na kupaa mbinguni, daima amejificha kutoka kwako kwa muda fulani, na kisha Anakuonekana kwa muda fulani. Anajifichua kwako kwa sababu ya haki yako, na Anakasirika na kuondoka kutoka kwako kwa sababu ya dhambi zako, kwa hiyo mbona huombi Kwake zaidi? Je, hukujua kwamba baada ya Pentekoste, Bwana Yesu Kristo ana agizo jingine duniani? Unajua tu ukweli kwamba Bwana Yesu Kristo alipata mwili, Akaja duniani, na kutundikwa msalabani. Hujawahi kutambua kwamba Yesu uliyemwamini awali amemwaminia mtu mwingine kazi Yake kitambo, na kwamba ilikamilishwa zamani, kwa hiyo Roho wa Bwana Yesu Kristo amekuja duniani tena katika mwili ili kufanya sehemu nyingine ya kazi Yake. Ningependa kusema kitu hapa—licha ya

ukweli kwamba kwa sasa mko katika mkondo huu, Ninaweza kusema kwamba wachache kati yenu wanamwamini mtu huyu kuwa Yule mliyepewa na Bwana Yesu Kristo. Mnajua tu kumfurahia; hamkiri kwamba Roho wa Mungu amekuja tena duniani, na hamkiri kwamba Mungu wa leo ndiye Yesu Kristo wa miaka mingi iliyopita. Na kwa hiyo Nasema kwamba ninyi nyote mnatembea pasi kuona—mnakubali tu popote mnapoishia—na hampi hili uzito hata kidogo. Kwa hiyo mnamwamini Yesu kwa maneno, lakini mnathubutu kumpinga Yule ambaye Mungu anamshuhudia leo bila kuficha. Je, si wewe ni mpumbavu? Mungu wa leo hajali kuhusu makosa yako. Hakushutumu. Unasema kwamba unamwamini Yesu, kwa hiyo Bwana wako Yesu Kristo anaweza kukuachilia? Je, unadhani kwamba Mungu ni pahali fulani pa wewe kutolea hisia, kudanganya na kusema uongo? Bwana wako Yesu Kristo anapojifichua mara nyingine, Ataamua iwapo wewe ni mwenye haki au iwapo wewe ni mwovu kwa msingi wa jinsi unavyotenda sasa. Watu wengi wanaishia kuwa na fikira kuhusu kile Ninachoita “ndugu Zangu,” na wanaamini kwamba mbinu za Mungu za kufanya kazi zitabadilika. Je, watu kama hawa hawakaribishi kifo? Je, Mungu anaweza kumshuhudia Shetani kama Mungu Mwenyewe? Je, humhukumu Mungu kwa kufanya hili? Je, unaamini kwamba mtu yeyote tu anaweza kuwa Mungu Mwenyewe? Ikiwa kweli ungejua, basi hungekuwa na fikira zozote. Kifungu kifuatacho kiko ndani ya Biblia: Vitu vyote ni kwa ajili Yake na vitu vyote vinatoka Kwake. Atawaleta wana wengi katika utukufu na Yeye ndiye Nahodha wetu.... Kwa hiyo hana aibu atuitapo ndugu. Huenda unaweza kuyakariri maneno haya kwa urahisi, lakini huelewi maana yake halisi. Je, humwamini Mungu pasi kuona?

Naamini kwamba kizazi chetu kimebarikiwa kuweza kuichukua njia ambayo vizazi vya awali havikuweza kukamilisha, na kutazama kuonekana tena kwa Mungu wa miaka mingi iliyopita—Mungu aliye miongoni mwetu, na Aliyejaa katika vitu vyote. Hungewahi kufikiri kwamba ungeitembea njia hii—je, hili ni jambo unaloliweza? Njia hii inaongozwa moja kwa moja na Roho Mtakatifu, inaongozwa na Roho wa Bwana Yesu Kristo aliyeongezwa nguvu mara saba, na ndiyo njia ambayo Mungu wa leo amekufungulia. Hata katika njozi zako zisizowezekana hungewahi kufikiria kwamba Yesu wa miaka mingi iliyopita angeonekana tena mbele yako. Je, huhisi mwenye furaha? Ni nani anayeweza kukutana ana kwa ana na Mungu? Mara nyingi huwa Nakiombea kikundi chetu kipokee baraka kubwa zaidi kutoka kwa Mungu, ili tuweze kufadhiliwa na Mungu na kupatwa na Yeye, lakini pia kumekuwa na nyakati nyingi ambapo Nimelia kwa uchungu kwa sababu yetu, nikimsihi Mungu atupe nuru, ili tuweze kutazama ufunuo mkubwa zaidi. Niwaonapo watu wanaojaribu kumpumbaza Mungu kila wakati na kamwe hawana hamu ya kufanikisha chochote, ama vinginevyo wanaojali mwili, au wanaojitahidi kwa ajili ya masilahi na sifa ili waonekane muhimu, Naweza kukosa kuhisi uchungu mkubwa moyoni Mwangu? Watu wanawezaje kuwa wapumbavu kiasi hicho? Kweli

kazi Yangu haijakuwa na matokeo? Ikiwa watoto wako wangekuasi na wakose kukupenda kama mzazi, ikiwa wangekosa dhamiri, ikiwa wangejijali tu na kamwe wasizingatie hisia zako, na wakufukuze kutoka nyumbani baada ya wao kukua, ungehisi vipi wakati huo? Je, si machozi yangetiririka usoni pako unapokumbuka damu, jasho na kujitolea ulivyotia katika kuwalea? Hivyo Nimemwomba Mungu mara nyingi na kusema, “Ee Mungu! Ni Wewe tu Ujuaye iwapo Ninaubeba mzigo kwa ajili ya kazi Yako. Mahali ambapo matendo Yangu hayalingani na mapenzi Yako, Unanifundisha nidhamu, Unanikamilisha, na kunifanya Nitambue. Ombi Langu la pekee Kwako ni kwamba Uwaguse watu hawa zaidi, ili Uweze kutukuzwa karibuni na waweze kupatwa na Wewe, ili kazi Yako iweze kutimiza mapenzi Yako, na mpango Wako uweze kukamilika mapema.” Mungu hataki kuwashinda watu kupitia kuwaadibu, Hataki siku zote kuwatawala watu kabisa. Anawataka watu watii maneno Yake na kufanya kazi kwa namna iliyo na nidhamu, na kwa kufanya hili, waridhishe mapenzi Yake. Lakini watu hawana aibu na wanamwasi kila wakati. Naamini kwamba ni bora kwetu kutafuta njia rahisi zaidi ya kumridhisha, yaani, kutii mipango Yake yote. Ikiwa kweli unaweza kutimiza hili, utakamilishwa. Je, hili si jambo rahisi na la furaha? Chukua njia unayopaswa kuchukua; usitilie maanani kile wanachosema wengine, na usifikirie sana. Je, si mustakabali na majaliwa yako viko mikononi mwako mwenyewe? Unajaribu daima kutoroka, ukitaka kuichukua njia ya dunia—lakini mbona huwezi kutoka? Kwa nini unasitasita katika njia panda kwa miaka mingi na kisha unaishia kuichagua njia hii tena? Baada ya kuzurura kwa miaka mingi, kwa nini sasa umerudi kwa hii nyumba bila kutaka? Je, haya ni mapenzi yako? Kwa wale kati yenu mlio katika mkondo huu, ikiwa hamniamini basi sikilizeni hili: Ikiwa umepanga kuondoka, ona kama Mungu atakuruhusu, ona jinsi Roho Mtakatifu anavyokugusa—lipitie mwenyewe. Kusema ukweli, hata ukipitia msiba, lazima uupitie katika mkondo huu, na kama kuna mateso, lazima uteseke hapa, leo; huwezi kuenda pengine. Je, unaelewa hili? Utaenda wapi? Hii ni amri ya Mungu ya utawala. Je, unafikiri kwamba Mungu kulichagua kundi hili la watu hakuna maana? Katika kazi Yake leo, Mungu hakasiriki kwa urahisi—lakini watu wakijaribu kuukatiza mpango Wake, uso Wake unabadilika mara moja, ukiacha kuwa mchangamfu na kugeuka wenye huzuni. Kwa hiyo, Nakushauri utulie na kutii mipango ya Mungu, na umruhusu Akukamilishe. Watu wanaofanya hili tu ndio werevu.

Njia ... (8)

Haijakuwa tu siku moja au mbili tangu Mungu aje duniani kushirikiana na wanadamu, kuishi na watu. Pengine, wakati huu wote watu wamemjua Mungu kwa kiwango fulani, na labda wamepata utambuzi muhimu wa kumhudumia Mungu, na wamepata uzoefu sana katika imani yao katika Mungu. Hata iweje, watu wanaelewa vizuri sana tabia ya Mungu, na maonyesho ya kila aina ya tabia za binadamu yanatofautiana kwa kweli. Jinsi Nionavyo, maonyesho

tofautitofauti ya watu yanatosha kwa Mungu kuyatumia kama sampuli, na shughuli zao za fikira zinatoshwa kwa Yeye kurejelea. Labda hii ni hali moja ambayo kwayo wanadamu hushirikiana na Mungu, ni ushirikiano usiokusudiwa wa mwanadamu na Mungu, ili utekelezaji huu unaoelekezwa na Mungu uwe wa kupendeza na wenye uhai, dhahiri sana. Ninasema mambo haya kwa ndugu zangu kama mwelekezaji mkuu wa mchezo huu wa kuigiza—kila mmoja wetu anaweza kunena na fikira na hisia zake baada ya kuliigiza hili, na kuzungumza kuhusu vile kila mmoja wetu anayapitia maisha yake ndani ya mchezo huu wa kuigiza. Huenda ikawa vyema kwa sisi kuwa na aina mpya kabisa ya kongamano ili kuifungua mioyo yetu na kuzungumza kuhusu sanaa yetu ya maonyesho, tuone vile Mungu atamwongoza kila mtu ili katika utambaji unaofuata tuweze kuonyesha kiwango cha juu zaidi cha sanaa yetu na kila mtu aweze kuigiza sehemu yake mwenyewe kwa kiasi kikuu zaidi iwezekanavyo, bila kutomridhisha Mungu. Natumai kwamba ndugu Zangu wataweza kulitilia hili maanani—hakuna anayeweza kulipuuza kwa sababu kuigiza sehemu fulani vizuri si jambo linaloweza kutimizwa katika siku moja au mbili. Linahitaji tuyapitie maisha na kuingia ndani kabisa katika maisha yetu halisi kwa kipindi kirefu, na kuwa na uzoefu wa utendaji wa aina mbalimbali za maisha. Ni wakati huo tu ndipo tunaweza kwenda juu ya jukwaa. Nimejawa tumaini kwa ajili ya ndugu Zangu, na Naamini kwamba hamjavunjika moyo wala kukata tamaa, na haijalishi kile ambacho Mungu anafanya, ninyi ni kama chungu chenye moto—huwa hamna uvuguvugu kamwe na mnaweza kushikilia mpaka mwisho, mpaka kazi ya Mungu ifichuliwe kwa ukamilifu, na mpaka mchezo wa kuigiza ambao Mungu anaelekeza ufike katika hitimisho la mwisho wake. Sina matakwa mengine kwenu. Kila Ninachotumai ni kwamba muweze kuendelea kushikilia, kwamba musiwe na wasiwasi kwa ajili ya matokeo, kwamba mshirikiane na Mimi ili kazi Ninayopaswa kufanya ifanyike vizuri, na kwamba hakuna atakayesababisha pingamizi au usumbufu. Sehemu hii ya kazi ikishatimizwa, Mungu atawafichulia ninyi kila kitu. Baada ya kazi Yangu kutimizwa, Nitawasilisha sifa njema yenu mbele ya Mungu kutoa maelezo Kwake. Je, hilo si bora? Tunaweza kusaidiana kutimiza malengo yetu wenyewe. Je, hili si suluhisho kamili kwa kila mtu? Huu ni wakati mgumu unaowahitaji mlipe gharama. Kwa sababu Mimi ndiye mwelekezi sasa, Natumai kwamba hakuna mmoja wenu aliyekerwa. Hii ndiyo kazi ambayo Ninafanya. Labda kutakuweco na siku moja ambapo Nitahamia kwa “kitengo cha kazi” cha kufaa na Nisifanye tena mambo yawe magumu kwenu. Nitawaonyesha ninyi chochote mnachopenda kuona, na pia Nitawakamilisha ninyi katika chochote mnachopenda kusikia. Lakini sio sasa—hii ni kazi ya leo na siwezi kuwapa uhuru kwa hulka zenu na kuwaruhusu kufanya chochote mnachotaka kufanya. Hivyo, kazi Yangu haingekuwa rahisi kufanya. Kusema kweli, hilo halingezea matunda yoyote na halingekuwa la manufaa kwenu. Kwa hiyo sasa mnahitaji “kupitia magumu,” na siku ifikapo ambapo hatua hii ya kazi Yangu itakuwa imetimizwa Nitakuwa huru. Sitaubeba mzigo mzito kama huu, na Nitakubali chochote mtakachoomba kutoka Kwangu; maadamu tu ni cha manufaa

kwa maisha yenu Nitatimiza maombi yenu. Nimechukua sasa jukumu zito. Siwezi kwenda kinyume cha amri za Mungu Baba, na Siwezi kuvuruga mipango ya kazi Yangu. Siwezi kusimamia mambo Yangu binafsi kupitia kwa mambo ya biashara Yangu. Natumai nyote mnaweza kunielewa na kunisamehe Mimi kwa sababu kila kitu Nifanyacho kinalingana na kusudi la Mungu Baba. Nafanya chochote Atakacho Nifanye haijalishi Anachotaka, na Siko radhi kuchochea hasira Yake au ghadhabu Yake. Mimi hufanya tu Ninachopaswa kufanya. Kwa hiyo kwa niaba ya Mungu Baba, Ninawashauri ninyi mvumilie tu kwa muda mrefu kidogo. Mtu yeyote asiwe na wasiwasi. Baada ya Mimi kutimiza Ninachotaka kufanya, mnaweza kufanya chochote mtakacho na kuona chochote mpendacho, lakini lazima Nitimize kazi Ninayohitaji kutimiza.

Katika hatua hii ya kazi sisi tunatakiwa kuwa na imani kuu na upendo mkuu. Huenda tukajikwaa kutokana na uzembe kidogo kabisa kwa sababu hatua hii ya kazi ni tofauti na zile zote za awali. Kile ambacho Mungu anakamilisha ni imani ya wanadamu—mtu hawezi kuiona au kuigusa. Kile ambacho Mungu anafanya ni kuyageza maneno kuwa imani, kuwa upendo, na kuwa uzima. Watu lazima wafikie kiwango ambacho wamestahimili mamia ya kusafisha na wawe na imani iliyo kuu zaidi kuliko ya Ayubu. Wanatakiwa kustahimili taabu ya ajabu sana na aina zote za mateso bila kuondoka kwa Mungu wakati wowote. Wanapokuwa watiifu hadi kufa, na wawe na imani kuu katika Mungu, basi hatua hii ya kazi ya Mungu imetimizwa. Ni kazi hii ndiyo Nimekubali kuifanya, kwa hiyo Natumai kwamba ndugu Zangu wanaweza kuelewa matatizo Yangu na hawana matakwa yoyote zaidi Kwangu. Haya ni matakwa ya Mungu Baba Kwangu na Siwezi kuepuka uhalisi huu. Lazima Nifanye kazi Ninayopaswa kufanya. Yote Ninayotumai ni kwamba msiwe bila busara, kwamba mpate utambuzi zaidi na msiyatazame masuala kwa urahisi sana. Fikira zenu ni za kitoto sana, za kijinga sana. Kazi ya Mungu sio rahisi kama mnavyoweza kufikiri, kwamba Anafanya tu chochote Atakacho kufanya. Ingekuwa hali ni hiyo mpango Wake ungeangamizwa. Hamngesema hivyo? Ninafanya kazi ya Mungu. Siwafanyii tu watu kazi zisizo za kawaida, kufanya chochote Ninachohisi kufanya na kupanga binafsi iwapo Nitafanya kitu au la. Sio rahisi vile sasa hivi. Nimetumwa na Baba kutenda kama mwelekezi—mnafikiri kwamba Nilipanga na kuchagua hili Mwenyewe? Maoni ya mwanadamu wakati mwingi yanaelekea kukatiza kazi ya Mungu, ndiyo maana, baada ya Mimi kufanya kazi kwa kipindi cha muda fulani, kuna maombi mengi kutoka kwa watu ambayo Sijaweza kutimiza na watu wote wamebadilisha mawazo yao kunihusu Mimi. Nyote mnapaswa kuelewa mawazo haya mliyonayo—Sina haja ya kuyataja moja kwa moja. Siwezi kufanya chochote ila kufafanua kazi Niifanyayo; hisia Zangu haziumizwi na hili katu. Mara tu mkishaelewa hilo, mnaweza kulichukulia vyovyote mtakavyo. Sitatoa pingamizi zozote kwa sababu hivi ndivyo Mungu hufanya kazi. Sishurutishwi kueleza yote. Nimekuja tu kutekeleza kazi ya maneno, kufanya kazi

na kuruhusu uigizaji huu uendelee kwa mwelekeo wa maneno. Sihitaji kusema mengi kuhusu mengine, na Siwezi kufanya jambo lingine lolote. Nimeeleza kila kitu Ninachotakiwa kusema. Chochote mnachofikiria kukihusu ni sawa, na haijalishi Kwangu. Lakini bado Ningependa kuwakumbusha ninyi kwamba kazi ya Mungu si rahisi kama mnavyoifikiria kuwa. Kadri isivyolingana na fikira za watu ndivyo umuhimu wake ulivyo wa kina, na kadri inavyolingana na fikira za watu, ndivyo isivyokuwa na thamani, na bila umuhimu halisi. Fikirieni maneno haya kwa makini—Nasema tu kitu hiki kimoja kuhusu hilo, na ninyi wenyewe mnaweza kuchambua mengine. Sitafanya ufafanuzi wowote.

Watu hufikiri kwamba Mungu hufanya mambo kwa njia fulani, lakini kwa mwaka huu uliopita au zaidi, je, kile ambacho tumeona na kupitia kuhusu kazi ya Mungu kimelingana kweli na fikira za binadamu? Tangu uumbaji wa ulimwengu mpaka sasa, hakuna hata mtu mmoja ambaye ameweza kugundua hatua au sheria za kazi ya Mungu. Ikiwa wangependa, ni kwa nini wale viongozi wa kidini hawatambui kwamba Mungu wakati wa sasa anafanya kazi kwa njia hii? Ni kwa nini watu wachache sana wanaelewa uhalisi wa leo? Kutokana na hili tunaweza kuona kwamba hakuna anayeielewa kazi ya Mungu—watu wanaweza tu kufanya mambo kulingana na uongozi wa Roho Wake, lakini hawawezi tu kutumia sheria kwa imara kwa kazi Yake. Ukichukua mfano na kazi ya Yesu na kuilinganisha na kazi ya Mungu ya sasa, ni kama vile watu wa Kiyahudi wakijaribu kumlinganisha Yesu na Yehova. Je, huku sio kupata hasara? Hata Yesu hakujua kazi ya Mungu katika siku za mwisho ingekuwa ipi; yote Aliyojua ni kwamba kile Alichohitaji kutimiza kilikuwa ni kazi ya kusulubiwa, kwa hiyo wengine wangependa? Wangependa ni kazi gani ambayo Mungu angeifanya katika siku za usoni? Mungu angefichua mipango Yake kwa wanadamu, ambao wamemilikiwa na Shetani? Je, huo si upumbavu? Kile ambacho Mungu anakuruhusu kujua na kuelewa ni mapenzi Yake. Hakuruhusu wewe ufikirie juu ya kazi Yake ya siku za usoni. Tunahitaji kujishughulisha tu na imani ndani ya Mungu, kutenda kwa mwongozo Wake kuwa wenye vitendo kwa utatuzi wa matatizo halisi na, na kutofanya mambo kuwa magumu kwa Mungu au kumletea Yeye matatizo. Tunapaswa tu kwenda kufanya tunachopaswa kufanya—maadamu tunaweza kuwa katika kazi ya Mungu ya wakati uliopo hiyo inatosha! Hii ni njia Ninayowaongoza nyinyi kwayo. Tunapaswa kuendelea mbele, na Mungu hatamtesa yeyote kati yetu. Katika mwaka huu uliopita wa uzoefu wenu wa ajabu mmepata mambo mengi sana; Naamini kwamba hamtafadhaishwa sana. Njia Ninayowaelekeza kwayo ni kazi Yangu, wajibu Wangu, na iliamriwa na Mungu kitambo sana ili tuweze kuamuliwa kabla kufika umbali huu, hadi leo—kwamba tumeweza kufanya hili ni baraka yetu kubwa, na ingawa haijakuwa njia rahisi, urafiki wetu ni wa milele, na utapitishwa moja kwa moja katika enzi. Kama zilikuwa nderemo na kicheko au huzuni na machozi, acha zote ziwe kumbukumbu nzuri! Yawezekana unajua kwamba siku za kazi Yangu ni chache. Nina miradi

mingi sana ya kazi, na Siwezi kuandamana nanyi mara kwa mara. Natumai mnaweza kunielewa Mimi—kwa sababu urafiki wetu wa asili bado uko vilevile. Labda siku moja Nitaonekana kwa mara nyingine mbele yenu, na Natumai kwamba hamtafanya mambo yawe magumu Kwangu. Hata hivyo, Mimi ni tofauti nanyi. Nasafiri kwenda kote kwa ajili ya kazi Yangu, na Siishi maisha Yangu kwa kupumzika tu kivivu katika hoteli nyingi. Bila kujali vile mlivyo, Mimi hufanya tu Ninachopaswa kufanya. Natumai kwamba mambo tuliyoshirikiana hapa awali yatakuwa kipeo cha uzuri wa urafiki wetu.

Inaweza kusemwa kwamba hii njia ilifunguliwa na Mimi, na kama ni chungu au tamu, Nimeiongoza njia. Kuweza kwetu kuendelea mpaka wakati wa sasa yote imekuwa ni kwa sababu ya neema ya Mungu. Huenda kukawa na wengine wanaonishukuru Mimi, na huenda kukawa na wengine wanaolalamika dhidi Yangu, lakini hakuna lililo muhimu kati ya hayo. Yote Nitakayo kuona ni kwamba kinachopaswa kutimizwa katika kundi hili la watu kimetimizwa. Hili linapaswa kusherehekewa. Kwa hiyo, sina kisasi dhidi ya wale wanaolalamika dhidi Yangu; yote Nitakayo ni kutimiza kazi Yangu haraka iwezekanavyo ili moyo wa Mungu uweze kuwa na raha hivi punde. Wakati huo Sitaubeba mzigo wowote mzito, na hakutakuwa na wasiwasi ndani ya moyo wa Mungu. Je, mko radhi kushirikiana kwa njia iliyo bora? Je, kufanya kazi ya Mungu vizuri sio lengo bora kwa ajili ya mapambano yetu? Inaweza kusemwa kweli kwamba tumepitia taabu nyingi na kupitia furaha na huzuni yote katika kipindi hiki cha wakati, na kwa jumla, utendaji wa kila mtu umekuwa takriban wa wastani. Labda, siku zijazo kutakuwa na kazi bora mtakayotakiwa kufanya, lakini msikawie katika kuwaza juu Yangu; fanyeni tu mnachopaswa. Ninachohitaji kufanya kinakaribia kufika mwisho, na Natumai kwamba mtakuwa waaminifu wakati wote na kwamba hamtakuwa wenye hamu ya mambo yaliyozeewa kuhusu kazi Yangu. Mnapaswa kujua kwamba Nimekuja tu kutimiza hatua moja ya kazi, bila shaka sio kufanya kazi yote ya Mungu. Hili ni jambo mnalotakiwa kuelewa. Msiwe na maoni mengine kulihusu. Kazi ya Mungu inahitaji njia nyingi zaidi ili iweze kukamilika; hamwezi kunitegemea Mimi kila mara. Labda mliona zamani sana kwamba Ninachofanya ni sehemu moja tu ya kazi hiyo; haimwakilishi Yehova au Yesu. Kazi ya Mungu imegawanywa katika hatua nyingi, kwa hivyo msiwe wagumu sana. Wakati Ninapofanya kazi lazima mnisikilize Mimi. Kazi ya Mungu imekuwa tofauti katika kila enzi moja; haibaki vilevile, na sio tu wimbo ule ule wa zamani unaoimbwa. Kuna kazi Yake ambayo ni ya kufaa kwa kila hatua na hubadilika pamoja na hatua hizo. Kwa vile umezaliwa katika enzi hii, lazima ule na kunywa maneno ya Mungu na kuyasoma maneno Yake. Siku huenda ikaja ambapo kazi Yangu itabadilika, ambapo kutokana nayo ni lazima mwendelee kwenda mbele jinsi mnavyopaswa kufanya. Kazi ya Mungu kamwe haiwezi kuwa na dosari. Ustilie maanani jinsi ulimwengu wa nje unavyobadilika; Mungu hawezi kuwa mwenye makosa na kazi Yake haiwezi kuwa yenye makosa. Ni kwamba tu wakati mwingine

kazi ya Mungu ya zamani hupita na kazi Yake mpya huanza; hata hivyo, haiwezi kusemwa kwamba kwa vile kazi mpya imekuja kazi ya zamani ni yenye makosa. Hiyo ni hoja ya uwongo! Kazi ya Mungu haiwezi kusemekana kuwa ni sahihi au yenye kosa, inaweza tu kusemekana kuwa ya mwanzoni au ya baadaye. Huu ni mwongozo wa imani ya watu katika Mungu na hauwezi bila shaka kupuuzwa.

Maoni Wanayopaswa Kushikilia Waumini

Ni kitu gani ambacho mwanadamu amepokea tangu alipomwamini Mungu mara ya kwanza? Umejua kitu gani kumhusu Mungu? Umebadilika kiasi gani kwa sababu ya imani yako kwa Mungu? Leo, nyote mnajua ya kwamba imani ya mwanadamu katika Mungu si kwa ajili ya wokovu wa roho na hali njema ya mwili tu, wala si kuimarisha maisha yake kwa njia ya upendo kwa Mungu, na kadhalika. Kama ilivyo sasa, kama unampenda Mungu kwa ajili ya ustawi wa mwili au furaha ya muda, basi hata kama, mwishoni, upendo wako kwa Mungu utafikia kilele chake na wewe hutautiliza kitu chochote, upendo huu unaoutafuta ni upendo mchafu na haumpendezi Mungu. Wale wanaotumia upendo kwa Mungu kusitawisha maisha yao yasiyopendeza na kujaza utupu katika mioyo yao ni wale ambao wanataka kuishi katika raha, si wale ambao kweli wanatafuta kumpenda Mungu. Upendo wa aina hii ni kinyume na matakwa ya mtu, harakati ya ridhaa ya hisia, na Mungu hahitaji upendo wa aina hii. Upendo wako, basi, ni upendo wa aina gani? Ni kwa ajili gani unampenda Mungu? Je, ni kiasi gani cha upendo wa kweli, ulicho nacho kwa Mungu sasa? Upendo wa watu wengi kati yenu ni kama uliotajwa hapo awali. Upendo wa aina hii unaweza tu kudumisha hali kama ilivyo; hauwezi kufikia uthabiti wa milele, wala kuchukua mizizi katika mtu. Aina hii ya upendo ni ule wa ua ambalo halizai matunda baada ya kuchanuka na hatimaye kunyauka. Kwa maneno mengine, baada ya wewe kumpenda Mungu mara moja kwa jinsi hii na hakuna mtu wa kukuongoza kwa njia ya mbele, basi utaanguka. Kama unaweza tu kumpenda Mungu katika wakati wa kumpenda Mungu na kutofanya mabadiliko katika tabia ya maisha yako baadaye, basi utaendelea kufunikwa na ushawishi wa giza, bila uwezo wa kutoroka, na bila uwezo wa kujinasua kwa kufungwa na kupumbazwa na Shetani. Hakuna mtu kama huyu anayeweza kukubaliwa na Mungu; mwishowe, roho zao, nafsi na mwili bado ni mali ya Shetani. Hili ni bila ya shaka. Wale wote ambao hawawezi kukubaliwa kikamilifu na Mungu watarudi mahali pao pa awali, yaani, kwa Shetani, na watakwenda chini kwa ziwa liwakalo moto wa jahanamu kukubali hatua ya pili ya adhabu kutoka kwa Mungu. Wale wanaokubaliwa na Mungu ni wale ambao wanamkataa shetani na kutoroka kutoka kwa miliki ya Shetani. Watu kama wale watahesabiwa rasmi miongoni mwa watu wa ufalme. Hivi ndivyo watu wa ufalme huja kuwa. Je, uko tayari kuwa mtu wa aina hii? Je, uko tayari kukubaliwa na Mungu? Je, uko tayari kutoroka kutoka miliki ya Shetani na kurudi kwa Mungu? Je, sasa wewe ni mali ya Shetani au umehesabiwa miongoni mwa watu wa ufalme?

Mambo hayo lazima yote yawe wazi na hayahitaji maelezo zaidi.

Katika nyakati zilizopita, watu wengi walifuatilia kwa jitihada na fikira za mwanadamu na kwa ajili ya matumaini ya mwanadamu. Mambo haya hayatajadiliwa sasa. La muhimu ni kupata njia ya kutenda ambayo itawezesha kila mmoja wenu kudumisha hali ya kawaida mbele ya Mungu na hatimaye kuvunja pingu za ushawishi wa Shetani, ili mpate kuwa wakubalika wa Mungu, na kuishi kwa kudhihirisha duniani matakwa ya Mungu kwenu. Ni haya tu yanayoweza kutimiza mapenzi ya Mungu. Wengi wanaamini katika Mungu, ila hawajui ni kitu gani Anachotamani Mungu wala ni nini anachotamani Shetani. Wao wanaamini kipumbavu na kuwafuata watu wengine kama vipofu, na kwa hivyo hawajakuwa kamwe na maisha ya kawaida ya Kikristo; hawana uhusiano wa kawaida wa binafsi na watu wengine, sembuse uhusiano wa kawaida ambao mwanadamu anao na Mungu. Kutoka kwa hili inaweza kuonekana kwamba matatizo na makosa ya mtu, na mambo mengine ambayo yanaweza kuzuia mapenzi ya Mungu ni mengi. Hili linatosha kuthibitisha kwamba mwanadamu bado hajaingia kwenye njia sahihi ya imani katika Mungu, wala hajaingia katika uzoefu halisi wa maisha ya binadamu. Hivyo, maana ya kuingia kwenye njia sahihi ya imani katika Mungu ni ipi? Kuingia kwenye njia iliyo sahihi ina maana kwamba unaweza kunyamazisha moyo wako mbele za Mungu wakati wote na kufurahia mawasiliano ya kawaida na Mungu, hatua kwa hatua ukipata kujua ni nini kinachokosa ndani ya mwanadamu na polepole kupata kumfahamu Mungu zaidi. Kwa njia hii, kila siku unapata maono mapya na kupata nuru kiroho; hamu yako inakua, na wewe kutafuta kuingia katika ukweli. Kila siku kuna mwanga mpya na ufahamu mpya. Kupitia njia hii, wewe hatua kwa hatua unavunja ushawishi wa Shetani na kuwa huru, na maisha yako yanakua kwa kiasi kikubwa. Mtu kama huyu ameweka mikakati ya kufuata mwenendo sawa. Tathmini uzoefu wako mwenyewe halisi na kuchunguza njia uliyoichukua katika imani yako kwa Mungu dhidi ya yaliyotajwa hapo juu. Wewe ni yule ambaye amepangwa kufuata mwenendo sawa? Ni katika masuala gani ambapo umejiweka huru kutokana na pingu za shetani na kutokana na ushawishi wa Shetani? Kama bado hujajiandaa kufuata njia iliyo sahihi, uhusiano wako na Shetani bado haujaisha. Kwa jinsi hiyo, ukimbizaji huu wa upendo kwa Mungu inaweza kusababisha upendo ambao ni sahihi, wa kujitolea, na safi? Unasema kwamba upendo wako kwa Mungu ni wa dhati na imara, bali hujajinasua kutoka kwa pingu za Shetani. Je, wewe si unajaribu kumpumbaza Mungu? Ukitaka kuufikia upendo safi kwa Mungu, kuwa wa Mungu kikamilifu, na kuwa mhesabiwa miongoni mwa watu wa ufalme, basi lazima kwanza ujiandae kufuata njia iliyo sahihi ya imani katika Mungu.

Kwenye Hatua za Kazi ya Mungu

Kutoka nje, inaonekana kwamba hatua za kazi ya sasa ya Mungu tayari zimekamilika, na

mwanadamu tayari amehukumiwa, kuadibiwa, kuangamizwa na kusafishwa na maneno ya Mungu, na amepitia hatua hizi kama majaribio ya watendaji huduma, usafishaji wa wakati wa kuadibu, majaribio ya kifo, majaribio ya foili^[a], na wakati wa kumpenda Mungu. Bado licha ya kupitia mateso makubwa katika kila hatua, watu wamebaki kutojua mapenzi ya Mungu. Kwa mfano, fikiria majaribio ya watendaji huduma: Bado hawaelewi kile walichopata, kile walichokuja kujua, na matokeo ambayo Mungu alitaka kutimiza. Tukiangalia kasi ya kazi ya Mungu, mwanadamu anaonekana hawezi kabisa kuwa sambamba na kasi ya leo. Inaweza kuonekana kwamba Mungu kwanza anamfichulia mwanadamu hatua hizi za kazi Yake leo, na kwamba badala ya kutimiza kiwango ambacho mwanadamu anafikiria kinawezekana katika zozote kati ya sehemu hizi, Anaangazia suala fulani. Kwa Mungu kumkamilisha mtu ili aweze kupatwa na Yeye kwa kweli, lazima Atekeleze hatua hizi zote zilizotajwa juu. Lengo la kufanya kazi hii ni kuonyesha ni hatua zipi ambazo Mungu lazima atekeleze ili Akamilishe kikundi cha watu. Hivyo, tukiangalia kutoka nje, hatua za kazi ya Mungu zimekamilika—lakini kimsingi, ndipo Ameanza tu rasmi kuwakamilisha mwanadamu. Watu wanapaswa kuelewa hili: Ni hatua za kazi Yake ambazo zimekamilika, lakini kazi yenyewe bado haijahitimika. Lakini katika dhana zao, watu huamini kwamba mwanadamu amefichuliwa hatua zote za kazi ya Mungu, na kwa hiyo hakuwezi kuwa na shaka kwamba kazi ya Mungu imekamilika. Njia hii ya kuyachukulia mambo ni yenye makosa kabisa. Kazi ya Mungu huenda kinyume na dhana za mwanadamu na huzipiga dhana kama hizi katika kila suala; hatua za kazi ya Mungu hasa ni tofauti na dhana za mwanadamu. Haya yote yanaonyesha hekima ya Mungu. Inaweza kuonekana kwamba dhana za mwanadamu zinasababisha vurugu mara kwa mara, na Mungu hukabili kila kitu ambacho mwanadamu hufikiria, jambo linalokuwa dhahiri wakati wa uzoefu halisi. Kila mtu hufikiri kwamba Mungu hufanya kazi haraka mno, na kwamba kazi ya Mungu hukamilika kabla ya wao kujua, kabla ya wao kupata ufahamu wowote na wakati ambapo bado wako katika hali ya kukanganywa. Hivyo ndivyo ilivyo katika kila hatua ya kazi Yake. Watu wengi sana huamini kwamba Mungu anawachezea watu—lakini hilo silo kusudi la kazi Yake. Mbinu Yake ya kufanya kazi ni ya kutafakari: kwanza kwa kuyakagua mambo kwa juu juu, kisha kuyachunguza kwa utondoti, na baada ya hapo kurekebisha maelezo haya kikamilifu—jambo ambalo huwapata watu wasipotarajia. Watu hujaribu kumdanganya Mungu, wakifikiri kwamba wakiendelea tu kuishi hadi kiwango fulani, Mungu ataridhishwa. Kwa kweli, Mungu anawezaje kuridhishwa na majaribu ya mwanadamu ya kuendelea kuishi? Ili kutimiza matokeo bora kabisa, Mungu hufanya kazi kwa kuwafumania watu, kwa kuchukua hatua wakati ambapo hawajui; hili huwapa ufahamu mkubwa zaidi wa hekima Yake, na ufahamu mkubwa zaidi wa haki na uadhama Wake na tabia Yake isiyokosewa.

Leo, Mungu ameanza rasmi kumkamilisha mwanadamu. Ili wafanywe wakamilifu, lazima

watu wapitie ufunuo, hukumu na kuadibiwa na maneno Yake, lazima wajaribiwe na kusafishwa na maneno Yake (kama vile majaribio ya watendaji huduma), na lazima waweze kuvumilia majaribio ya kifo. Maana ya hili ni kwamba wakiwa katikati ya hukumu, kuadibu na majaribio ya Mungu, mtu anayetenda mapenzi ya Mungu kweli anaweza kutoa sifa kutoka katika kina cha moyo wake katikati ya hukumu, kuadibu na majaribu ya Mungu, mtu mkamilifu yuko hivi, na hii hasa ndiyo kazi ambayo Mungu ananuia kufanya, na kazi ambayo Atakamilisha. Watu hawapaswi kufanya uamuzi kuhusu mbinu ambazo kwazo Mungu hufanya kazi bila kufikiria. Wanapaswa tu kufuatilia kuingia katika maisha. Hili ni jambo la muhimu. Usichunguze mbinu ya kazi ya Mungu daima; hili litazuia tu matarajio yako ya baadaye. Umeona kiasi kipi cha mbinu ambayo kwayo Mungu anafanya kazi? Umekuwa mtiifu kiasi kipi? Umpata kiasi kipi kutoka kila kwa mbinu ya kazi Yake? Je, uko radhi kukamilishwa na Mungu? Je, ungetaka kukamilishwa? Haya yote ni mambo ambayo unapaswa kuyaelewa vizuri na kuyaingia.

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Mwanadamu Mpotovu Hawezi Kumwakilisha Mungu

Binadamu amekuwa akiishi katika funiko la ushawishi wa giza, huku akiwa amezuiliwa bila ya kuachiliwa na ushawishi wa Shetani. Nayo tabia ya binadamu, baada ya kutengenezwa na Shetani, inaendelea kuongezeka kuwa potovu. Mtu anaweza kusema kwamba binadamu huishi daima na tabia yake potovu ya kishetani, asiweze kumpenda Mungu kwa kweli. Kwa sababu ya hili, kama binadamu anataka kumpenda Mungu, lazima anyang'anywe kujidai kwake, kujigamba, kiburi, majivuno, na sifa nyingine kama hizo zinazomilikiwa na tabia ya Shetani. La sivyo, upendo wake si safi, ni upendo wa kishetani, na ule ambao hauwezi kabisa kupokea idhini ya Mungu. Kama binadamu hakamilishwi, kushughulikiwa, kuvunjwa, kupogolewa, kufundishwa nidhamu, kuadibiwa, au kusafishwa na Roho Mtakatifu moja kwa moja, hakuna yeyote anayeweza kumpenda Mungu kwa kweli. Ukisema kwamba sehemu ya tabia yako inamwakilisha Mungu na hivyo basi unaweza kumpenda Mungu kwa kweli, basi wewe ndiwe unayezungumza maneno ya kiburi na ni binadamu wa upuuzi. Binadamu kama hao ni malaika mkuu! Asili ya ndani ya binadamu haiwezi kumwakilisha Mungu kwa njia ya moja kwa moja. Lazima binadamu aiondoe asili yake ya ndani kupitia kwa ukamilifu wa Mungu, na kisha kupitia kutunza na kutosheleza mapenzi ya Mungu tu, na hata zaidi kupitia kwa kazi ya Roho Mtakatifu, ndipo kuishi kwa kudhihirishwa kwake kunaweza kuidhinishwa na Mungu. Hakuna anayeishi katika mwili anayeweza kumwakilisha Mungu kwa njia ya moja kwa moja isipokuwa kama yeye ni binadamu anayetumiwa na Roho Mtakatifu. Hata hivyo, hata kama huyu, tabia yake na kile anachoishi kwa kudhihirisha chote hakiwezi kuchukuliwa kwamba kinamwakilisha Mungu

kabisa; inaweza kusemekana tu kwamba kile anachoishi kwa kudhihirishwa kinatawaliwa na Roho Mtakatifu. Tabia ya mtu kama huyo haiwezi kumwakilisha Mungu.

Ingawa tabia ya binadamu inaamrisha na Mungu—hili halina shaka na linaweza kuchukuliwa kama jambo zuri—limetengenezwa na Shetani. Hiyo ndiyo maana tabia zote za binadamu kwa kweli ni tabia ya Shetani. Mtu anaweza kusema kuwa Mungu, katika tabia yake, ni mnyofu katika kutekeleza mambo, na kwamba yeye pia anatenda kwa njia hii; yeye pia anatabia kama hii, na hivyo basi anasema kwamba tabia yake inamwakilisha Mungu. Huyu ni binadamu wa aina gani? Je, tabia potovu ya kishetani inaweza kumwakilisha Mungu? Yeyote yule anayetangaza kwamba tabia yake ni wakilishi kwa Mungu, huyo mtu anamkufuru Mungu na kumtukana Roho Mtakatifu! Tukiangalia namna ambavyo Roho Mtakatifu hufanya kazi, kazi ambayo Mungu anafanya hapa ulimwenguni ni kwa ajili ya kushinda pekee. Hii ndiyo maana, nyingi ya tabia potovu za kishetani za binadamu bado hazijatakaswa, na ndiyo maana mienendo ya maisha ya binadamu bado ni taswira ya Shetani. Ndicho binadamu huamini kuwa chema a na kinawakilisha vitendo vya mwili wa binadamu au kwa usahihi zaidi, kinawakilisha Shetani na hakiwezi kumwakilisha Mungu kabisa. Hata kama binadamu tayari anampenda Mungu hadi kufikia kiwango ambacho anaweza kufurahia maisha ya mbinguni hapa ulimwenguni, anaweza kutamka kauli kama vile: “Eh Mungu! Siwezi kukupenda vya kutosha,” na kwamba amefikia eneo la juu zaidi, huwezi kusema kwamba anaishi kwa kumdhihirisha Mungu au kumwakilisha Mungu, kwani kiini cha binadamu ni tofauti na kile cha Mungu. Binadamu hawezi kamwe kuishi kwa kumdhihirisha Mungu, sembuse kuwa Mungu. Kile ambacho Roho Mtakatifu anamwelekeza binadamu kuishi kwa kudhihirisha ni kulingana tu na kile ambacho Mungu anahitaji kutoka kwa binadamu.

Vitendo vyote na matendo ya Shetani vinaonyeshwa kupitia kwa binadamu. Sasa vitendo vyote na matendo yote ya binadamu ni maonyesho ya Shetani na hivyo basi haviwezi kumwakilisha Mungu. Binadamu ni mfano halisi wa Shetani, na tabia ya mwanadamu haiwezi kuiwakilisha tabia ya Mungu. Baadhi ya wanadamu ni wenye tabia nzuri; Mungu anaweza kufanya baadhi ya kazi kupitia kwa tabia hiyo nayo kazi yao inatawaliwa na Roho Mtakatifu. Ilhali tabia yao haiwezi kumwakilisha Mungu. Kazi ambayo Mungu hufanya ndani yao ni kule tu kufanya kazi na pamoja na kupanua kile ambacho tayari kimo ndani yao. Wawe ni manabii au binadamu wanaotumiwa na Mungu kutoka kwa enzi zilizopita, hakuna yeyote anayeweza kumwakilisha Mungu moja kwa moja. Binadamu wote huja kumpenda Mungu kwa sababu tu ya shurutisho kutoka kwa mazingira yao, na hakuna kati yao ambaye hujitahidi kushiriki kwa hiari yake. Mambo mema ni yapi? Yote ambayo hutoka kwa njia ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu ni mema. Hata hivyo, tabia ya binadamu imetengenezwa na Shetani na haiwezi kumwakilisha Mungu. Ni Mungu mwenye mwili tu—mapenzi Yake, nia Yake ya kuteseka, haki,

utiifu, unyenyekevu na kujificha Kwake—hivi vyote humwakilisha Mungu moja kwa moja. Hii ni kwa sababu Alipokuja, Hakuwa na asili ya dhambi na alikuja moja kwa moja kutoka kwa Mungu bila ya kutengenezwa na Shetani. Yesu yumo tu katika mfano wa mwili wenye dhambi na hawakilishi dhambi; kwa hivyo, vitendo Vyake, matendo na maneno, mpaka wakati ule kabla ya mafanikio Yake ya kazi kupitia kwa kusulubishwa (pamoja na kusulubishwa) vyote ni viwakilishi vya moja kwa moja vya Mungu. Mfano wa Yesu unatosha kuthibitisha kwamba binadamu yeyote aliye na asili ya dhambi hawezi kumwakilisha Mungu, na kwamba dhambi ya binadamu inamwakilisha Shetani. Hiyo ni kusema kwamba dhambi haimwakilishi Mungu na Mungu hana dhambi. Hata kazi inayofanywa ndani ya binadamu na Roho Mtakatifu inaweza tu kuchukuliwa kuwa imetawaliwa na Roho Mtakatifu na haiwezi kusemwa kwamba ilifanywa na binadamu kwa niaba ya Mungu. Lakini kwa kadiri ambavyo binadamu anahusika, si dhambi yake wala tabia yake inamwakilisha Mungu. Kwa kuangalia kazi ambayo Roho Mtakatifu amefanya ndani kwa mwanadamu kutoka zamani hadi sasa, mtu anaona kwamba mwanadamu anacho kile anachoishi kwa kudhihirisha kwa sababu Roho Mtakatifu amefanya kazi juu yake. Ni wachache sana wanaoweza kuishi kwa kudhihirisha ukweli baada ya kushughulikiwa na kufundishwa nidhamu na Roho Mtakatifu. Ambayo ni kusema kwamba, kazi ya Roho Mtakatifu tu ndiyo iliyopo; ushirikiano kwa upande wa binadamu haupo. Je, unaliona suala hili kwa uwazi zaidi sasa? Kwa hiyo basi, ni nini unachofaa kufanya ili kufanya kazi kwa bidii pamoja na Yeye huku Roho Mtakatifu akiwa kazini na, kwa kufanya hivyo, kutimiza wajibu wako?

Njia ya Huduma ya Kidini Lazima Ipigwe Marufuku

Tangu mwanzo wa kazi Yake katika ulimwengu mzima, Mungu amewaamulia kabla watu wengi kumhudumia, wakiwemo watu kutoka kila tabaka la maisha. Kusudio Lake ni kutimiza mapenzi Yake mwenyewe na kuhakikisha kwamba kazi Yake hapa ulimwenguni inatimia kwa urahisi. Hili ndilo kusudio la Mungu katika kuwachagua watu wa kumhudumia. Kila mtu anayemhudumia Mungu lazima aelewe mapenzi haya ya Mungu. Kupitia kazi hii Yake, watu wanaweza kuona vizuri zaidi hekima ya Mungu na kudura ya Mungu, na kuona kanuni za kazi Yake hapa ulimwenguni. Mungu kwa kweli anakuja ulimwenguni kufanya kazi Yake, kuwasiliana na watu, ili nao waweze kuona vizuri zaidi matendo Yake. Leo, kundi hili la watu lina bahati kubwa kwa kundi hili lenu kumhudumia Mungu wa utendaji. Hii ni baraka isiyopimika kwenu. Kwa kweli ni Mungu anayewainua. Katika kumteua mtu ili amhudumie, Mungu siku zote huwa na kanuni Zake binafsi. Kumhudumia Mungu hakika, kama vile watu wanavyofikiria, si suala tu la kuwa na shauku. Leo mnaona kwamba mtu yeyote anayeweza kumhudumia Mungu akiwa mbele Yake anafanya hivyo kwa sababu wana mwongozo wa Mungu na kazi ya Roho Mtakatifu, na kwa sababu wao ni watu wanaofuata ukweli. Haya ndiyo mahitaji ya kiwango cha chini zaidi ambayo wote wanaomhudumia Mungu wanapaswa kuwa

nayo.

Kumtumikia Mungu si kazi rahisi. Wale ambao tabia yao potovu haibadiliki hawawezi kamwe kumhudumia Mungu. Kama tabia yako haijahukumiwa na kuadibiwa na neno la Mungu, basi tabia yako bado inamwakilisha Shetani. Hii inatosha kuthibitisha kwamba huduma yako kwa Mungu ni kutokana na nia yako nzuri wewe binafsi. Ni huduma inayotokana na asili yako ya kishetani. Unamhudumia Mungu na hulka yako ya kiasili, na kulingana na mapendeleo yako ya kibinafsi; na zaidi, unaendelea kufikiria kwamba Mungu anapenda chochote kile unachopenda kufanya, na kwamba Mungu anachukia chochote kile ambacho hupendi kufanya, na unaongozwa kabisa na mapendeleo yako binafsi katika kazi yako. Je, huku kunaweza kuitwa kumhudumia Mungu? Hatimaye tabia yako ya maisha haitabadilishwa hata chembe; badala yake, utakuwa msumbufu hata zaidi kwa sababu umekuwa ukimhudumia Mungu, na hii itafanya tabia yako potovu kukita mizizi zaidi. Kwa njia hii, utaendelea kwa ndani sheria kuhusu huduma kwa Mungu zitokanazo kimsingi na hulka yako binafsi, na uzoefu unaotokana na kuhudumu kwako kulingana na tabia yako binafsi. Hili ni funzo kutokana na uzoefu wa kibinadamu. Ni falsafa ya binadamu ya kuishi katika dunia. Watu kama hawa ni wa Mafarisayo na wale wajumbe wa kidini. Kama hawatawahi kuzinduka na kutubu, basi hakika watageuka na kuwa wale Makristo wa uwongo na wapinga Kristo watakaowadanganya watu katika siku za mwisho. Makristo wa uwongo na wapinga Kristo waliozungumziwa watainuka kutoka miongoni mwa watu kama hawa. Kama wale wanaomhudumia Mungu watafuata hulka yao na kutenda kulingana na mapenzi yao binafsi, basi wamo katika hatari ya kutupwa nje wakati wowote. Wale wanaotumia miaka yao mingi ya uzoefu kwa kumhudumia Mungu ili kutega mioyo ya watu, kuwasomea na kuwadhibiti, kujiinua wao wenyewe—na wale katu hawatubu, katu hawakiri dhambi zao, katu hawakatai manufaa ya cheo—watu hawa wataanguka mbele ya Mungu. Hawa ni watu walio kama Paulo, waliojaa majivuno ya vyeo vyao na wanaoonyesha ukubwa wao. Mungu hatawakamilisha watu kama hawa. Aina hii ya huduma huzuia kazi ya Mungu. Watu wanapenda kushikilia vitu vya kale. Wanashikilia fikira za kale, wanashikilia vitu vya kale. Hiki ni kizuizi kikuu katika huduma yao. Kama huwezi kuvitupa vitu hivi, vitu hivyo vitayakaba maisha yako yote. Mungu hatakupongeza, hata kidogo, hata kama utaivunja miguu yako au mgongo wako ukitia bidii, au hata ukifa katika “huduma” ya Mungu. Kinyume cha mambo ni kwamba: Atasema kwamba wewe ni mtenda maovu.

Kufikia leo, Mungu atawakamilisha kirasmi wale wasiokuwa na fikira za kidini, ambao wako tayari kuweka pembeni nafsi zao za kale, na ambao wanamtii tu Mungu kwa moyo wa kawaida, na kuwafanya kuwa watimilifu wale wanaotamani neno la Mungu. Watu hawa wanafaa kusimama na kumhudumia Mungu. Kwake Mungu kunayo hekima nyingi na isiyoisha. Kazi Yake ya kustaajabisha na matamshi Yake yenye thamani vinasubiri hata idadi kubwa ya watu

waweze kuvifurahia. Kama ilivyo sasa, wale walio na fikira za kidini, wanaochukua hali ya ukubwa, na wale ambao hawawezi kujiweka pembeni wanaona vigumu sana kukubali vitu hivi vipya. Hakuna fursa ya Roho Mtakatifu kuwakamilisha watu hawa. Kama mtu hajaamua kutii, na hana kiu ya neno la Mungu, basi mtu huyo hataweza kupokea mambo mapya. Wataendelea tu kuwa waasi zaidi na zaidi, kuwa wajanja zaidi na zaidi, na hatimaye kujipata kwenye njia mbaya. Katika kufanya kazi Yake sasa, Mungu atawainua watu zaidi wanaompenda kwa kweli na wanaoweza kukubali mwangaza mpya. Na Atakatiza kabisa maafisa wa kidini wanaoonyesha ukubwa wao. Wale wanaokataa mabadiliko kwa ukaidi: Hataki hata mmoja wao. Je, unataka kuwa mmoja wa watu hao? Je, unatekeleza huduma yako kulingana na mapendeleo yako, au unafanya kile Mungu anachotaka? Hili ni jambo ambalo lazima ujijulie mwenyewe. Je, wewe ni mmojawapo wa maafisa wa kidini, au wewe ni mtoto mchanga anayefanywa kuwa mtimilifu na Mungu? Je, ni kiwango kipi cha huduma yako ambacho kinapongezwa na Roho Mtakatifu? Ni kiwango kipi ambacho Mungu hatasumbuka kukumbuka? Baada ya miaka mingi ya huduma, maisha yako yamebadilika kiasi kipi? Je, uko wazi kuhusu mambo haya yote? Kama unayo imani ya kweli, basi utaweka pembeni fikira zako za kale za kidini na utamhudumia Mungu kwa njia bora zaidi na kwa njia mpya. Hujachelewa sana kusimama sasa. Fikira za kale za kidini zitayakaba maisha ya mtu. Uzoefu ambao mtu anapata utamwongoza mbali na Mungu, kufanya mambo kwa njia yake mwenyewe. Usipoviweka vitu hivi chini, vitakuwa kikwazo katika kukua kwa maisha yako. Mungu siku zote amewakamilisha wote wanaomhudumia. Hawatupilii mbali kwa urahisi tu. Kama tu utakubali kwa kweli hukumu na kuadibu kwa neno la Mungu, kama unaweza kuweka pembeni matendo yako na sheria za kidini za kale, na kukoma kutumia fikira za kale za kidini kama kipimo cha neno la Mungu hii leo, ni hapo tu ndipo kutakuwa na mustakabali kwako. Lakini kama utashikilia vitu vya kale, kama bado unavithamini, basi huwezi kupata wokovu. Mungu hawatambui watu kama hao. Kama kweli unataka kukamilishwa, basi lazima uamue kutupilia mbali kabisa kila kitu cha kale. Hata kama kile kilichokuwa kimefanywa awali kilikuwa sahihi, hata kama ilikuwa ni kazi ya Mungu, ni lazima bado uweze kuiweka pembeni na uache kuishikilia. Hata kama ilikuwa kazi ya Roho Mtakatifu iliyo wazi, iliyofanywa moja kwa moja na Roho Mtakatifu, leo lazima uiweke pembeni. Hufai kuishikilia. Hili ndilo Mungu anahitaji. Kila kitu lazima kifanywe upya. Katika kazi ya Mungu na neno la Mungu, Harejelei vitu vya kale ambavyo vilishapita, na vilevile Hafukui historia ya kale. Mungu siku zote ni mpya na kamwe si mzee. Hashikilii hata maneno Yake mwenyewe ya kitambo inayoonyesha kwamba Mungu hafuati mafundisho ya dini yoyote. Katika hali hii, kama mwanadamu, kama siku zote unashikilia kabisa vitu vya kale, ukikataa kuviachilia na kuvitumia kwa njia ya fomyula, huku naye Mungu hafanyi kazi tena katika njia Alizokuwa akifanya awali, basi maneno yako na matendo yako siyo ya kukatiza? Je, hujawa adui wa Mungu? Je, uko radhi kuyaacha maisha yako yote yaharibike kwa sababu ya mambo haya ya kale? Mambo haya ya

kale yatakufanya kuwa mtu anayezuia kazi ya Mungu. Je, mtu kama huyo ndiye wewe unataka kuwa? Kama kweli hutaki kuwa hivyo, basi acha mara moja kile unachofanya na ubadilike; anza tena upya. Mungu hakumbuki huduma yako ya kale.

Katika Imani Yako kwa Mungu Unapaswa Kumtii Mungu

Kwa nini unamwamini Mungu? Watu wengi wanafadhaishwa na swali hili. Siku zote wana mitazamo tofauti kuhusu Mungu wa vitendo na Mungu wa mbinguni, jambo linaloonyesha kwamba wanamwamini Mungu sio ili wamtii, bali kupata manufaa fulani, au kuepuka mateso ya janga. Wakati huo tu ndipo wanakuwa watiifu kwa kiasi fulani, lakini utii wao ni wa masharti, ni kwa ajili ya matarajio yao wenyewe, na kushinikiziwa. Hivyo: kwa nini unamwamini Mungu? Ikiwa ni kwa ajili ya matarajio yako tu, na majaliwa yako, basi ni bora zaidi usingeamini. Imani kama hii ni kujidanganya, kujihakikishia, na kujishukuru. Kama imani yako haijajengwa katika msingi wa utii kwa Mungu, basi hatimaye utaadhibiwa kwa kumpinga Mungu. Wale wote ambao hawatafuti utii kwa Mungu kwa imani yao wanampinga Mungu. Mungu anaomba kwamba watu watafute ukweli, kwamba wawe na kiu ya neno la Mungu, na wanakula na kunywa maneno ya Mungu, na kuyaweka katika matendo, ili waweze kupata utii kwa Mungu. Kama motisha zako ni hizo kweli, basi Mungu atakuinua juu hakika, na hakika Atakuwa mwenye neema kwako. Hakuna anayeweza kutilia shaka hili, na hakuna anayeweza kulibadilisha. Ikiwa motisha zako sio kwa ajili ya utii kwa Mungu, na una malengo mengine, basi yote ambayo unasema na kufanya—maombi yako mbele ya Mungu, na hata kila tendo lako—litakuwa linampinga Mungu. Unaweza kuwa unaongea kwa upole na mwenye tabia ya upole, kila tendo lako na yale unayoyaonyesha yanaweza kuonekana ni sahihi, unaweza kuonekana kuwa mtu anayetii, lakini linapofikia suala la motisha zako na mitazamo yako juu ya imani kwa Mungu, kila kitu unachofanya kipo kinyume cha Mungu, na ni uovu. Watu wanaoonekana watii kama kondoo, lakini mioyo yao inahifadhi nia mbovu, ni mbwa mwitu katika ngozi ya kondoo, wanamkosea Mungu moja kwa moja, na Mungu hatamwacha hata mmoja. Roho Mtakatifu atamfichua kila mmoja wao, ili wote waweze kuona kwamba kila mmoja wa hao ambao ni wanafiki hakika watachukiwa na kukataliwa na Roho Mtakatifu. Usiwe na shaka: Mungu atamshughulikia na kumkomesha kila mmoja.

Kama huwezi kukubali nuru mpya ya Mungu, na huwezi kuelewa yote ambayo Mungu anayafanya leo, na huyafuati, au unayatilia shaka, unayahukumu, au unayachunguza na kuyachambua, basi huna akili ya kuweza kumtii Mungu. Kama, nuru ya hapa na sasa inatokea, na bado unathamini nuru ya jana na kuipinga kazi mpya ya Mungu, basi wewe si chochote zaidi ya mtu mpumbavu—wewe ni mmoja wa wale wanaompinga Mungu kwa makusudi. Jambo muhimu katika kumtii Mungu ni kuitambua nuru mpya, na kuweza kuikubali na kuiweka katika

vitendo. Huu pekee ndio utii wa kweli. Wale ambao hawana hiari ya kuwa na kiu ya Mungu hawana uwezo wa kuwa na akili ya kumtii Mungu, na wanaweza tu kumpinga Mungu kama matokeo ya kuridhika kwao na jinsi hali ilivyo. Kwamba mtu hawezi kumtii Mungu ni kwa sababu amefungwa na kitu kilichotangulia kabla. Mambo ambayo yalikuja kabla yamewapatia watu kila namna ya dhana na njozi za uongo kuhusu Mungu ambazo zimekuwa ndiyo taswira ya Mungu akilini mwao. Hivyo, kile wanachoamini ni dhana zao wenyewe, na viwango vya mawazo yao wenyewe. Ikiwa utampima Mungu ambaye anafanya kazi halisi leo dhidi ya Mungu wa mawazo yako mwenyewe basi imani yako inatoka kwa Shetani, na ni kulingana na mapendeleo yako mwenyewe—na Mungu hataki imani kama hii. Bila kujali sifa zao ni za juu sana kiasi gani, na bila kujali kujitoa kwao—hata kama wamejitoa jitihada za maisha yao yote katika kazi Yake, na wamejitoa mhanga—Mungu hakubali imani yoyote kama hii. Anawaonyesha tu neema kidogo, na kuwaacha waifurahie kwa muda. Watu kama hawa hawawezi kuuweka ukweli katika vitendo, Roho Mtakatifu hafanyi kazi ndani yao, na badala yake Mungu atamwondoa kila mmoja wao. Bila kujali ama ni wazee au vijana, wale ambao hawamtii Mungu katika imani yao na wana motisha mbaya, ni wale ambao wanapinga na kuingilia, na watu kama hao bila kuhoji wataondolewa na Mungu. Wale ambao hawana utii kwa Mungu hata kidogo, ambao wanalitambua tu jina la Mungu, na wana ufahamu kiasi juu ya mapenzi na wema wa Mungu lakini hawaenendi sawa na hatua za Roho Mtakatifu na hawatii kazi na maneno ya sasa ya Roho Mtakatifu—watu kama hao wanaishi katikati ya neema ya Mungu, na hawatachukuliwa na kukamilishwa na Mungu. Mungu huwakamilisha watu kupitia utii wao, kupitia kula kwao, kunywa na kufurahia maneno ya Mungu, na kupitia mateso na usafishaji maishani mwao. Ni kupitia tu imani kama hii ndipo tabia za watu zinaweza kubadilika, baada ya hapo tu ndipo wanaweza kuwa na maarifa ya kweli kuhusu Mungu. Kutoridhika na kuishi katikati ya neema za Mungu, kuwa na kiu ya ukweli, na kutafuta ukweli, na kunuia kuchumwa na Mungu—hii ndio maana ya kumtii Mungu katika hali ya utambuzi; hii ndiyo aina ya imani ambayo Mungu anataka. Watu ambao hawafanyi kitu zaidi ya kufurahia neema za Mungu hawawezi kukamilishwa, au kubadilishwa, na utii wao, uchaji Mungu, na upendo na ustahimilivu vyote hivyo ni vya juujuu tu. Wale ambao wanafurahia tu neema za Mungu hawawezi kumfahamu Mungu kweli, na hata pale wanapomjua Mungu, maarifa yao ni ya juujuu, na wanasema mambo kama vile Mungu anampenda mwanadamu, au Mungu ni mwenye huruma kwa mwanadamu. Hii haiwakilishi maisha ya mwanadamu, na haionyeshi kwamba kweli watu wanamjua Mungu. Ikiwa, maneno ya Mungu yatakapowasafisha, au majaribu yake yatakapowajia, watu hawataweza kumtii Mungu—ikiwa, badala yake, watakuwa watu wa mashaka na kuanguka chini—basi hawana utii hata kidogo. Ndani yao, kuna kanuni na masharti mengi kuhusu imani kwa Mungu, uzoefu wa zamani ambao ni matokeo ya miaka mingi ya imani, au mafundisho mbalimbali kutoka kwenye Biblia. Je, watu kama hawa wanaweza

kumwamini Mungu? Watu hawa wamejawa na mambo ya wanadamu—wanawezaje kumtii Mungu? Wote wanatii kulingana na mapendeleo yao binafsi—je, Mungu anaweza kutamani utii kama huu? Huku sio kumtii Mungu bali ni kufungamanishwa na mafundisho, ni kujiridhisha na kujifariji mwenyewe. Ikiwa unasema kwamba huu ni utii kwa Mungu, je, hivi hutakuwa unamkufuru Yeye? Wewe ni Farao wa Misri, unafanya uovu, unajishughulisha katika kazi ya kumpinga Mungu—je, Mungu anaweza kutaka kazi kama hii? Ni bora ungefanya haraka ukatubu na kuweza kujitambua kiasi fulani. Ikiwa sivyo, ni bora uende nyumbani: hivyo itakuwa imekusaidia sana kuliko huduma yako kwa Mungu, hutaingilia wala kusumbua, utakuwa umeijua sehemu yako, na kuishi vizuri—na hiyo haitakuwa bora zaidi? Kwa namna hiyo utakuwa umeepuka kumpinga Mungu na kuweza kuadhibiwa!

Ni Muhimu Sana Kuanzisha Uhusiano wa Kawaida na Mungu

Watu wanaamini katika Mungu, wanampenda Mungu, na kumkidhi Mungu kwa kugusa Roho wa Mungu kwa moyo wao, hivyo kupata ridhaa ya Mungu; na wakati wanajihusisha na maneno ya Mungu kwa moyo wao, kwa hivyo wanasisimuliwa na Roho wa Mungu. Ikiwa unataka kufikia maisha ya kawaida ya kiroho na kuanzisha uhusiano wa kawaida na Mungu, basi lazima kwanza umpe Yeye moyo wako, na kuutuliza moyo wako mbele za Mungu. Ni baada tu ya kuumimina moyo wako mzima kwa Mungu ndipo unaweza kuingia hatua kwa hatua katika maisha ya kiroho yanayostahili. Kama, kwa imani yao katika Mungu, watu hawautoi moyo wao kwa Mungu, ikiwa moyo wao hauko katika Mungu, na wala hawauchukulii mzigo wa Mungu kama wao wenyewe, basi kila kitu wanachofanya ni kumdanganya Mungu, nayo ni matendo ya watu wa kidini, wasioweza kuipokea sifa ya Mungu. Mungu hawezi kupata kitu chochote kutoka kwa aina hii ya mtu; aina hii ya mtu anaweza tu kutumika kama foili^[a] kwa kazi ya Mungu, kama pambo katika nyumba ya Mungu, kuchukua nafasi, naye hana manufaa—Mungu hamtumii aina hii ya mtu. Katika mtu kama huyo, sio tu kwamba hakuna nafasi kwa ajili ya kazi ya Roho Mtakatifu, hata zaidi hakuna thamani ya ukamilifu; aina hii ya mtu ni “mfu atembeaye” halisi—hana sehemu ambazo zinaweza kutumika na Roho Mtakatifu—wao wote wametwaliwa na Shetani, kupotoshwa kwa kiwango kilichokithiri na Shetani, ambao ni chombo cha kuondolewa na Mungu. Kwa sasa, katika kuwatumia watu, Roho Mtakatifu hatumii tu hizo sehemu zao zinazopendeza ili kufanikisha mambo, pia Anazikamilisha na kuzibadilish sehemu zao zisizopendeza. Kama moyo wako unaweza kumiminwa ndani ya Mungu, na kukaa kimya mbele za Mungu, basi utakuwa na nafasi na sifa za kuhitimu ili kutumiwa na Roho Mtakatifu, kupokea nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu, na hata zaidi, utakuwa na nafasi kwa Roho Mtakatifu kufidia dosari zako. Unapompa Mungu moyo wako, katika upande chanya, unaweza kupata uingiaji wa kina zaidi na ufikie kiwango cha juu zaidi cha uelewaji; katika upande hasi, utakuwa na uelewa zaidi wa makosa na dosari zako mwenyewe, utakuwa na hamu zaidi ya kutafuta

kuyakidhi mapenzi ya Mungu, na hutakuwa katika hali ya kukaa tu, utaingia ndani kwa utendaji. Hii itamaanisha kuwa wewe ni mtu sahihi. Katika kigezo cha kwamba moyo wako uko shwari mbele za Mungu, jambo muhimu kama unapokea sifa kutoka kwa Roho Mtakatifu au la na kama unampendeza Mungu au la ni kama unaweza kuingia ndani kwa utendaji. Wakati Roho Mtakatifu anampa mtu nuru na anamtumia mtu, Hamfanyi hasi kamwe, lakini mara zote Humfanya aendeleo kwa utendaji. Hata kama ana udhaifu, anaweza kutoishi kulingana nao, anaweza kuepukana na kuchelewesha kukuza maisha yake, naye kutafuta kuyakidhi mapenzi ya Mungu. Hiki ni kiwango. Ukiweza kufikia hili, ni thibitisho la kutosha kwamba mtu ameupata uwepo wa Roho Mtakatifu. Ikiwa mtu yuko hasi daima, na hata baada ya kupata nuru ili kujijua bado yuko hasi na wa kukaa tu, bila uwezo wa kusimama na kutenda pamoja na Mungu, basi aina hii ya mtu anaipokea tu neema ya Mungu, bali Roho Mtakatifu hayuko naye. Mtu akiwa hasi, hii inamaanisha kuwa moyo wake haujamgeukia Mungu na roho yake haijaguswa na Roho wa Mungu. Hii inapaswa kutambuliwa na wote.

Katika uzoefu wako unaona kuwa moja ya masuala muhimu zaidi ni kuutuliza moyo wako mbele ya Mungu. Ni suala ambalo linahusu maisha ya kiroho ya watu, na kuendelea kwa maisha yao. Ni kama tu moyo wako uko na amani mbele za Mungu ndio kutafuta kwako ukweli na mabadiliko katika tabia yako kutazaa matunda. Kwa sababu unakuja ukiwa na mizigo mbele za Mungu na huwa unahisi kila mara kuwa unapungukiwa kiasi kikubwa, kwamba kuna ukweli mwingi ambao unahitaji kujua, uhalisi mwingi unaohitaji kupitia, na kwamba unapaswa kujali kikamilifu kuhusu mapenzi ya Mungu—mambo haya kila mara huwa mawazoni mwako, ni kana kwamba yamekufinyia chini sana kiasi kwamba huwezi kupumua, na hivyo unahisi mzito wa moyo (lakini sio kwa hali hasi). Ni watu wa aina hii pekee ndio wanastahili kukubali kupata nuru ya maneno ya Mungu na kuguswa na Roho wa Mungu. Ni kwa sababu ya mzigo wao, kwa sababu ni wenye moyo mzito, na, inaweza kusemwa, kwa sababu ya gharama ambayo wamelipa na mateso ambayo wamepitia mbele ya Mungu ndio wanapata nuru na mwangaza wa Mungu, kwa kuwa Mungu hamtendei yeyote kwa upendeleo. Yeye huwa mwenye haki kila mara katika kuwatendea watu, lakini Yeye sio holela katika kuwakimu watu, na hawapi bila masharti. Huu ni upande mmoja wa tabia Yake yenye haki. Katika maisha halisi, watu wengi bado hawajaufikia ulimwengu wa aina hii. Kwa kiwango cha chini zaidi, mioyo yao bado haijamgeukia Mungu kikamilifu, na hivyo bado hakujakuwa na mabadiliko yoyote makubwa katika tabia ya maisha yao. Hii ni kwa sababu wanaishi tu kati ya neema ya Mungu, na bado hawajapata kazi ya Roho Mtakatifu. Vigezo vya Mungu kuwatumia watu ni kama ifuatavyo: Mioyo yao inamgeukia Mungu, wanasumbuliwa na maneno ya Mungu, wanakuwa na mioyo ya kutamani, na wako na azimio la kutafuta ukweli. Ni watu wa aina hii tu ndio wanaoweza kupata kazi ya Roho Mtakatifu na mara kwa mara wapate nuru na mwangaza. Watu ambao Mungu huwatumia

huonekana kwa nje kama watu wasio na akili na kama wasio na uhusiano wa kawaida na wengine, ingawa wao huzungumza na adabu, hawazungumzi kiholela, na wanaweza daima kuwa na moyo uliotulia mbele ya Mungu. Lakini ni mtu wa aina hiyo tu ndiye anatosha kutumiwa na Roho Mtakatifu. Mtu huyu asiye na akili anayezungumziwa na Mungu huonekana kama asiye na uhusiano wa kawaida na wengine, na hana upendo wa kuelekea nje au matendo ya juu juu, lakini anapokuwa akieleza mambo ya kiroho anaweza kufungua roho yake na kwa kujinyima awatolee wengine mwangaza na nuru ambayo amepata kutoka kwa uzoefu wake wa hakika mbele za Mungu. Hivi ndivyo anavyodhihirisha upendo wake kwa Mungu na kuridhisha mapenzi ya Mungu. Wengine wote wanapokuwa wanamkashifu na kumdhihaki, ana uwezo wa kutoelekezwa na watu wa nje, matukio, au vitu, na bado anaweza kutulia mbele za Mungu. Mtu wa aina hii inavyooneka yuko na utambuzi wake mwenyewe wa pekee. Bila kujali wengine, moyo wake kamwe haumwachi Mungu. Wengine wanapokuwa wakizungumza kwa furaha na kwa vichekesho, moyo wake bado unasalia mbele za Mungu, kutafakari neno la Mungu au kusali kwa kimya kwa Mungu aliye moyoni mwake, akitafuta makusudi ya Mungu. Kamwe hawatilii maanani udumishaji wa uhusiano wa kawaida na wengine. Mtu wa aina hii inavyoonekana hana falsafa ya maisha. Kwa nje, mtu huyu ni mchangamfu, anayependwa, asiye na hatia, lakini pia anamiliki hisia ya utulivu. Huu ni mfano wa mtu ambaye Mungu anamtumia. Mambo kama falsafa ya kuishi au “mantiki ya kawaida” hayawezi kufanya kazi kwa mtu wa aina hii; mtu wa aina hii ameutoa moyo wake wote kwa neno la Mungu, ambaye anaonekana kuwa na Mungu tu katika moyo wake. Hii ni aina ya mtu ambaye Mungu anamrejelea kama mtu “bila mantiki,” naye tu ni mtu ambaye anatumiwa na Mungu. Alama ya mtu ambaye anatumiwa na Mungu ni: Haijalishi ni lini au wapi, moyo wake daima uko mbele za Mungu, na haijalishi jinsi gani wengine ni wenye anasa, jinsi gani wanavyoshiriki katika tamaa, wanajiingiza katika anasa za kimwili—moyo wake kamwe haumwachi Mungu, naye hafuatani na umati. Aina hii ya mtu pekee ndiye anafaa kwa ajili ya matumizi ya Mungu, naye hasa ni yule ambaye amekamilika na Roho Mtakatifu. Ikiwa huwezi kufikia hatua hii, basi hustahili kupatwa na Mungu, ili kukamilishwa na Roho Mtakatifu.

Ikiwa unataka kuwa na uhusiano wa kawaida na Mungu, basi lazima moyo wako umgeukie Mungu. Hili likiwa msingi, pia utakuwa na uhusiano wa kawaida na watu wengine. Iwapo huna uhusiano wa kawaida na Mungu, basi haijalishi unachofanya kudumisha uhusiano wako na watu wengine, haijalishi jinsi gani unafanya kazi kwa bidii au ni nguvu kiasi gani unaweka ndani yake, bado ni ya falsafa ya mwanadamu ya maisha. Unadumisha nafasi yako miongoni mwa watu kupitia mtazamo wa mwanadamu na falsafa ya mwanadamu ili kwamba watu wakupe wewe sifa, lakini hufuati neno la Mungu ili kuanzisha uhusiano wa kawaida na watu. Iwapo huzingatii uhusiano wako na watu lakini unadumisha uhusiano wa kawaida na Mungu, ikiwa uko

tayari kumpa Mungu moyo wako na ujifunze kumtii, basi kwa kawaida sana, uhusiano wako na watu wote utakuwa wa kawaida. Kwa njia hii, uhusiano huu haujengwi kwa mwili, bali juu ya msingi wa upendo wa Mungu. Kwa kiasi kikubwa hakuna ushirikiano uliojengwa juu ya mwili, lakini katika roho kuna ushirikiano na vilevile upendo, starehe, na kutoleana kwa wenza. Haya yote yanafanywa kwa msingi wa moyo unaomridhisha Mungu. Uhusiano huu haudumishwi kwa kutegemea falsafa ya mwanadamu ya maisha, bali unaundwa kwa kawaida kupitia mzungu wa Mungu. Hauhitaji jitihada zilizofanywa na binadamu. Unahitaji tu kutenda kulingana na maadili ya neno la Mungu. Je, unayo hiari ya kuwa mwenye kufikiria mapenzi ya Mungu? Je, uko tayari kuwa mtu “bila mantiki” mbele za Mungu? Je, uko tayari kuutoa moyo wako kwa Mungu kabisa, na kutofikiri kuhusu msimamo wako kati ya watu? Kati ya watu wote ambao una mawasiliano nao, ni gani ambao kati yao unayo mahusiano bora zaidi? Wepi kati yao ambao unayo mahusiano mabaya zaidi nao? Je, mahusiano yako na watu ni ya kawaida? Je, unawachukulia watu wote kwa usawa? Je, uhusiano wako na wengine umeimarishwa kwa mujibu wa falsafa yako ya maisha, ama umejengwa kwenye msingi wa upendo wa Mungu? Wakati mtu hautoi moyo wake kwa Mungu, basi roho yake inakuwa butu, inakufa ganzi na kutofahamu. Mtu wa aina hii kamwe hataelewa maneno ya Mungu na kamwe hatakuwa na uhusiano wa kawaida na Mungu; tabia ya mtu wa aina hiikamwe haitabadilika. Kubadilisha tabia ya mtu ni mchakato wa mtu kuutoa kabisa moyo wake kwa Mungu, na wa kupokea nuru na mwangaza kutoka kwa maneno ya Mungu. Kazi ya Mungu inaweza, kumruhusu mtu kuingia kwa utendaji, na pia kumwezesha kuepuka masuala yake hasi baada ya kupata maarifa. Unapoweza kuutoa moyo wako kwa Mungu, utaweza kuhisi kila harakati yenye hila ndani ya roho yako, nawe utajua kila nuru na mwangaza upokelewao kutoka kwa Mungu. Shikilia hili, nawe utaingia katika njia ya kukamilishwa na Roho Mtakatifu hatua kwa hatua. Kadri moyo wako unavyoweza kuwa mtulivu mbele za Mungu, ndivyo roho yako itakavyokuwa makini zaidi na wa kutaka uangalifu mkubwa, na kadri roho yako itakavyoweza kutambua kuchochewa na Roho Mtakatifu, kisha uhusiano wako na Mungu utakuwa wa kawaida zaidi na zaidi. Uhusiano wa kawaida kati ya watu huundwa juu ya msingi wa kumpa Mungu mioyo yao haufanikishwi kupitia jitihada za binadamu. Bila Mungu miyoni mwao, uhusiano kati ya watu ni uhusiano wa mwili tu. Sio uhusiano wa kawaida, lakini badala yake, ni utelekezaji kwa ajili ya tamaa za mwili. Ni uhusiano ambao Mungu anachukia, Asiupenda. Ukisema kuwa roho yako imeguzwa, lakini daima unataka kuwa na ushirika na watu wanaokupendeza, na wale unaowachukulia kwa hali ya juu, na iwapo kuna mtafutaji mwingine ambaye hakupendezi, ambaye huna upendeleo kwake na huwezi kujihusisha naye, huu ni ushahidi zaidi kuwa wewe uko chini ya hisia zako na kuwa huna uhusiano wa kawaida na Mungu kamwe. Unajaribu kumdanganya Mungu na kuficha ubaya wako mwenyewe. Hata ingawa unaweza kushirikisha uelewano kiasi lakini unabeba ubaya moyoni mwako, kila kitu unachofanya ni kizuri tu kwa kiwango cha mwanadamu. Mungu

hatakusifu—unatenda kulingana na mwili, sio kulingana na mzigo wa Mungu. Iwapo unaweza kuutuliza moyo wako mbele ya Mungu na kuwa na ushirikiano wa kawaida na wale wote wanaompenda Mungu, ni hapo tu ndipo utakuwa uko tayari kwa matumizi ya Mungu. Kwa njia hii, haijalishi jinsi unavyopatana na wengine, haitakuwa kulingana na falsafa ya maisha, lakini itakuwa kuishi mbele ya Mungu, kuufikiria mzigo Wake. Je, ni watu wangapi wa aina hii wapo miongoni mwenu? Je, mahusiano yako na watu wengine ni ya kawaida kweli? Yamejengwa katika msingi upi? Je, ni falsafa ngapi za maisha zimo ndani mwako? Je, zimetupiliwa mbali? Ikiwa moyo wako hauwezi kumgeukia Mungu kabisa, basi wewe si wa Mungu—unatoka kwa Shetani, na mwishowe utarudishwa kwa Shetani. Wewe hustahili kuwa mmoja wa watu wa Mungu. Yote haya yanahitaji kufikiria kwako kwa makini.

Tanbihi:

a. “Foili” inahusu mtu au kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Maisha Ya Kawaida ya Kiroho Huwaongoza Watu Kwenye Njia Sahihi

Mmetembea tu sehemu ndogo sana ya njia ya muumini katika Mungu, na bado hamjaingia kwenye njia sahihi, kwa hiyo bado mko mbali na kutimiza kiwango cha Mungu. Hivi sasa, kimo chenu hakitoshi kuyakidhi mahitaji Yake. Kwa sababu ya ubora wenu wa tabia na vilevile asili yenu ya maumbile ya upotovu, nyinyi daima huichukulia kazi ya Mungu kwa uzembe na hamuichukulii kwa uzito. Hii ni dosari yenu kubwa zaidi. Zaidi ya hayo, hamwezi kuipata njia ya Roho Mtakatifu. Wengi wenu hamuifahamu na hamwezi kuiona kwa dhahiri. Zaidi ya hayo, wengi wenu hamtilii maanani suala hili, na hata hamlichukulii kwa uzito. Mkiendelea kufanya hivi na msipoiua kazi ya Roho Mtakatifu, basi njia ambayo mnaichukua kama muumini katika Mungu itakuwa bure. Hii ni kwa sababu hamfanyi kila liwezekanalo ili kutafuta kutimiza mapenzi ya Mungu, na pia kwa sababu hamshirikiani vizuri na Mungu. Sio kwamba Mungu hajawafanyia kazi, au kwamba Roho Mtakatifu hajawasisimua. Ni kuwa nyinyi ni wazembe sana kiasi kwamba hamuichukulii kazi ya Roho Mtakatifu kwa uzito. Lazima mbadilike mara moja na kutembea njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu. Hii ndiyo mada kuu ya leo. “Njia hii inayoongozwa na Roho Mtakatifu” ni ili watu wapate nuru katika roho zao, wawe na ufahamu wa neno la Mungu, wapate ufahamu kuhusu njia iliyo mbele yao, na waweze kuingia katika ukweli hatua kwa hatua, na kuja kumwelewa Mungu zaidi na zaidi. Njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu hasa ni kwamba watu wawe na ufahamu zaidi wa neno la Mungu, bila mikengeuko na kuelewa kubaya, ili waweze kutembea ndani yake. Ili kutimiza athari hii, mtahitaji kufanya kazi kwa upatanifu na Mungu, kutafuta njia sahihi ya kutia katika vitendo, na kutembea katika njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu. Hii inahusu ushirikiano kwa upande wa mwanadamu, yaani,

mnachofanya kutimiza mahitaji ya Mungu kwenu, na jinsi mnavyotenda ili kuingia katika njia sahihi ya imani katika Mungu.

Inaonekana kuwa changamano sana kutembea kwenye njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu, lakini utatambua kuwa mchakato huu ni rahisi zaidi ikiwa njia ya kutenda ni dhahiri kabisa kwako. Ukweli ni kwamba watu wana uwezo wa yote ambayo Mungu anahitaji kutoka kwao—Yeye hajaribu kumfunza nguruwe kuimba. Katika hali zote, Mungu hutafuta kutatua matatizo ya watu na kusuluhisha mahangaiko yao. Nyinyi nyote lazima muelewe hili; msimuelewe Mungu vibaya. Njia ya Roho Mtakatifu ni kulitumia neno la Mungu kuwaongoza watu. Kama ilivyotajwa hapo awali, lazima mpeane mioyo yenu kwa Mungu. Hili ni sharti la kutembea kwenye njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu. Lazima mfanye hili ili muingie kwenye njia sahihi. Mtu anawezaje kumpa Mungu moyo wake kwa kusudi? Mnapopitia kazi ya Mungu na kumwomba katika maisha yenu ya kila siku, ninyi hufanya hivyo kwa uzembe—ninyi humwomba Mungu huku mkifanya kazi. Je, huku kunaweza kuitwa kumpa Mungu mioyo yenu? Mnafikiria kuhusu mambo ya nyumbani au shughuli za mwili; ninyi daima mna nia mbili. Je, hili linaweza kufikiriwa ni kuituliza mioyo yenu mbele za Mungu? Hii ni kwa sababu moyo wako daima umetawaliwa na tamaa ya mambo ya nje, na hauwezi kumgeukia Mungu. Ikiwa mnataka kweli kuifanya mioyo yenu kuwa na amani mbele za Mungu, lazima mfanye kazi ya ushirikiano kwa makusudi. Hiyo ni kusema, kila mmoja wenu lazima achukue muda kuwa mbali na kila mtu, jambo, na chombo kwa ajili ya ibada zenu binafsi za kiroho, ambapo mtaweza kuleta amani kwa mioyo yenu na kujituliza mbele za Mungu. Mnapaswa kuwa na muhtasari wenu binafsi wa ibada ambapo mnaweza kurekodi ufahamu wenu wa neno la Mungu na jinsi roho zenu zimesisimuliwa, haijalishi kama mnachoandika ni cha kina au ni cha juujuu. Tulizeni mioyo yenu mbele za Mungu kwa kusudi. Ikiwa unaweza kutoa saa moja au mbili kwa maisha ya kiroho ya kweli wakati wa mchana, basi maisha yako siku hiyo yatahisi kusitawishwa na moyo wako utakuwa mchangamfu na bila hatia. Ikiwa unaishi maisha haya ya kiroho kila siku, basi utaweza kumpa Mungu moyo wako zaidi na zaidi, roho yako itakuwa imara zaidi na zaidi, hali yako itakuwa bora zaidi na zaidi, utakuwa na uwezo zaidi wa kutembea katika njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu, na Mungu atakupata baraka zaidi na zaidi. Lengo la maisha yenu ya kiroho ni kutafuta kwa makusudi na kupata kuwepo kwa Roho Mtakatifu. Sio kuzingatia sheria au kufanya taratibu za dini, bali kutenda kweli pamoja na Mungu na kudhibiti miili yenu. Hiki ndicho mwanadamu anapaswa kufanya, kwa hiyo lazima mtumie juhudi zenu zote ili kufanya hivi. Kadri unavyoshirikiana bora zaidi na kadri unavyojitahidi zaidi, ndivyo utakavyoweza zaidi kugeuza moyo wako kwa Mungu, na ndivyo utakavyozidi kutuliza moyo wako mbele Yake. Mara tu utakapofikia hali fulani, Mungu ataupata moyo wako kabisa. Hakuna atakayeweza kuyumbisha au kuuteka moyo wako, na utakuwa wa Mungu kabisa. Ikiwa

unatembea katika njia hii, neno la Mungu litajifichua kwako wakati wote na kukupa nuru kwa kila kitu ambacho huelewei—hii yote inaweza kutimizwa kwa sababu ya ushirikiano wako. Hii ndiyo maana Mungu daima husema, “Wote wanaofanya kazi pamoja na Mimi, Nitawatuza mara mbili.” Lazima muone njia hii kwa dhahiri. Ikiwa mnataka kutembea katika njia sahihi, basi lazima mfanye yote muwezayo kumridhisha Mungu. Lazima mfanye yote muwezayo kufikia maisha ya kiroho. Mwanzoni, huenda usiweze kutimiza mengi katika suala hili, lakini usijiruhusu kurudi nyuma au kugaagaa katika ukanaji—lazima uendeleo kufanya kazi kwa bidii! Kadri unavyoishi maisha ya kiroho, ndivyo moyo wako utakavyomilikiwa zaidi na maneno ya Mungu, ukishughulika na mambo haya daima na kuubeba mzigo huu daima. Baada ya hiyo, unaweza kufichua ukweli wako wa ndani kabisa kwa Mungu kupitia maisha yako ya kiroho, mwambie unachotaka kufanya, kile ambacho umekuwa ukifikiri, ufahamu wako na maoni yako mwenyewe ya neno la Mungu. Usizuie chochote, hata kidogo! Jizoeze kuzungumza maneno yaliyo ndani ya moyo wako kwa Mungu, mwambie ukweli, na usisite kuzungumza yaliyo moyoni mwako. Kadri unavyofanya hivi, ndivyo utakavyohisi zaidi upendo wa Mungu, na moyo wako utavutiwa zaidi na zaidi kumwelekea Mungu. Wakati ambapo hili litafanyika, utahisi kwamba Mungu ni mpenzi zaidi kwako kuliko mtu mwingine yeyote. Hutawahi kumwacha Mungu kamwe, lolote liwalo. Ikiwa utafanya aina hii ya ibada ya kiroho kila siku na usiiondoe akilini mwako, bali uichukulie kama wito wako katika maisha, basi neno la Mungu litaumiliki moyo wako. Hii ndiyo maana ya kuguswa na Roho Mtakatifu. Itakuwa kana kwamba moyo wako daima umetawaliwa na Mungu, kana kwamba kumekuwa na upendo ndani ya moyo wako daima. Hakuna anayeweza kuliondoa hilo kutoka kwako. Wakati hili litatokea, Mungu ataishi ndani yako kweli na kuwa na nafasi ndani ya moyo wako.

Ahadi kwa Wale Ambao Wamekamilishwa

Ni njia gani ambayo Mungu hutumia kumkamilisha mwanadamu? Ni vipengele vipi vinavyojumuishwa? Je, uko tayari kukamilishwa na Mungu? Je, uko tayari kukubali hukumu na kuadibu kwa Mungu? Unajua nini kuhusu maswali haya? Kama huwezi kuzungumzia maarifa kama haya, basi hii inaonyesha kwamba bado huijui kazi ya Mungu na hujapatiwa nuru katu na Roho Mtakatifu. Binadamu wa aina hii hawezi kukamilishwa. Wanaweza tu kupokea kiasi kidogo cha neema ili kufurahia kwa muda mfupi na haiwezi kuendelezwa kwa kipindi kirefu. Kama mtu hufurahia tu neema ya Mungu, hawezi kukamilishwa na Mungu. Baadhi wanaweza kutoshelezwa na amani na furaha ya mwili, maisha yenye furaha bila ya dhiki au msiba, huku wakiishi kwa amani na familia zao bila ya mapigano au ugomvi. Wanaweza hata kuamini kwamba hii ni baraka ya Mungu, lakini kwa kweli, ni neema ya Mungu tu. Hamwezi kutosheka tu kwa kufurahia neema ya Mungu. Kufikiria kwa aina hii ni kuchafu mno. Hata ukisoma neno la Mungu kila siku, uombe kila siku, na roho yako ihisi furaha na amani halisi, ilhali mwishowe

huwezi kuzungumzia maarifa yoyote ya Mungu na kazi Yake au hujapata uzoefu wa mambo kama hayo, na haijalishi ni kiasi gani cha neno la Mungu ambacho umekula na kunywa, ukihisi tu amani na furaha katika roho yako na kwamba neno la Mungu ni tamu mno kiasi kwamba haliwezi kulinganishwa na kingine chochote, kana kwamba huwezi kulifurahia ukatosheka, lakini huna uzoefu halisi na huna hakika yoyote na neno la Mungu, basi ni nini unachoweza kupokea kutoka kwa aina hii ya imani katika Mungu? Kama huwezi kuishi kwa kudhihirisha kiini cha neno la Mungu, kula na kunywa kwako kwa maneno ya Mungu na maombi vyote vinahusu dini. Basi binadamu wa aina hii hawezi kukamilishwa na hawezi kupatwa na Mungu. Wale wote waliopatwa na Mungu ni wale wanaofuatilia ukweli. Kile ambacho Mungu hufaidi si mwili wa binadamu wala miliki zake, lakini sehemu iliyo ndani yake inayomilikiwa na Mungu. Kwa hivyo, Mungu huukamilisha moyo wa binadamu wala si mwili wake, ili moyo wa binadamu uweze kupatwa na Mungu. Kwa maneno mengine, kiini cha kusema kwamba Mungu humkamilisha mwanadamu ni kwamba Mungu huukamilisha moyo wa mwanadamu ili uweze kumgeukia Mungu na kumpenda Yeye.

Mwili wa binadamu hufa. Haifaidi chochote kwa Mungu kuupata mwili wa binadamu, kwani ndio ule ule ambao bila shaka huoza. Hauwezi kupokea urithi wa Mungu au baraka Zake. Kama Mungu anaupata tu mwili wa binadamu na kuuhifadhi mwili wa binadamu katika mfululizo huu, binadamu atakuwa katika mfululizo huu kwa jina tu, lakini moyo wa binadamu ungemilikiwa na Shetani. Basi binadamu hangeweza tu kuwa maonyesho ya Mungu, bali badala yake angekuwa mzigo Wake. Kwa hivyo Mungu kuchagua binadamu hakungekuwa na maana. Wale watakaokamilishwa na Mungu ni wale watakaopokea baraka za Mungu na urithi Wake. Yaani, wanasikia na kuelewa kile Mungu Alichio nacho na Alichio, ili kiwe kile ambacho walichio nacho ndani yao; wanayo maneno yote ya Mungu ndani yao; haijalishi ni vipi nafsi ya Mungu ilivyo, mnaweza kusikia na kuelewa kila kitu Anachokuambia vile kilivyo, na hivyo kuishi kwa kudhihirisha ukweli. Huyu ndiye aina ya binadamu aliyekamilishwa na Mungu na aliyepatwa na Mungu. Binadamu wa aina hii tu ndiye anayestahili kurithi baraka hizi alizofadhiliwa na Mungu:

1. Kupokea upendo mzima wa Mungu.
2. Kutenda kulingana na mapenzi ya Mungu katika kila kitu.
3. Kupokea mwongozo wa Mungu, kuishi chini ya mwangaza wa Mungu, na kupatiwa nuru na Mungu.
4. Kuishi kwa kudhihirisha taswira inayopendwa na Mungu hapa ulimwenguni; kumpenda Mungu kwa kweli kama vile Petro alivyofanya, kusulubishwa kwa sababu ya Mungu na kustahili kufa kwa kuufidia upendo wa Mungu; kuwa na utukufu sawa na Petro.

5. Kupendwa, kuheshimiwa, na kuvutiwa na wote ulimwenguni.

6. Kushinda utumwa wote wa kifo na Kuzimu, kutoipatia fursa yoyote kazi ya Shetani, kumilikiwa na Mungu, kuishi ndani ya roho safi na changamfu, na kutokuwa na hisia zozote za uchovu.

7. Kuwa na hisia isiyoelezeka ya msisimko na furaha siku zote katika maisha yako yote, ni kana kwamba ameona kuja kwa siku ya utukufu wa Mungu.

8. Kupokea utukufu pamoja na Mungu, na kuwa na sura inayofanana na watakatifu wapendwa wa Mungu.

9. Kuwa kile ambacho Mungu anapenda zaidi ulimwenguni, yaani, mwana mpendwa wa Mungu.

10. Kubadilisha maumbile na kupaa juu pamoja na Baba kwenye mbingu ya tatu, na kuuzidi mwili.

Wale tu wanaoweza kurithi baraka za Mungu ni wale waliokamilishwa na Mungu na kupatwa na Mungu. Je, umefaidi chochote? Mungu amekukamilisha hadi kiwango gani? Mungu hamkamilishi binadamu bila mpango. Kunayo masharti na matokeo dhahiri yanayoweza kuonekana na binadamu. Si jinsi mwanadamu anavyoamini, kwamba mradi tu awe na imani katika Mungu, anaweza kukamilishwa na kupatwa na Mungu, na anaweza kupokea hapa ulimwenguni baraka na urithi wa Mungu. Mambo kama haya ni magumu mno, na hata zaidi inapohusu kubadilika kwa taratibu. Kwa sasa, kile ambacho mnafaa kutafuta kimsingi ni kukamilishwa na Mungu katika mambo yote, na kukamilishwa na Mungu kupitia kwa watu wote, mambo yote na vitu vyote ambavyo mnakumbwa navyo, ili mambo zaidi ya kile Mungu Alichio yatashirikishwa ndani yenu. Lazima kwanza mpokee urithi wa Mungu ulimwenguni kabla ya kustahili kurithi baraka nyingi na kubwa zaidi kutoka kwa Mungu. Mambo yote haya ndiyo ambayo mnafaa kutafuta na ambayo kwanza mnafaa kuelewa. Zaidi unavyotafuta kukamilishwa na Mungu katika mambo yote, ndivyo utakavyoweza kuona mkono wa Mungu zaidi katika mambo yote, na hivyo kutafuta kwa bidii kuingia katika hali ya neno la Mungu na uhalisia wa neno Lake kupitia mitazamo tofauti na katika mambo tofauti. Huwezi kutosheka na hali hasi kama kutotenda dhambi tu, au kutokuwa na dhana, kutokuwa na filosofia ya kuishi, na kutokuwa na hiari ya binadamu. Mungu humkamilisha mwanadamu kwa njia tofauti, na inawezekana katika mambo yote kwako kukamilishwa hatimaye. Huwezi tu kukamilishwa kwa kuzingatia mambo halisi, lakini pia mambo hasi, na hivyo kuboresha kile unachopata. Kila siku kunazo fursa za kukamilishwa na muda wa kupatwa na Mungu. Baada ya kipindi cha kupitia mambo kama haya, utabadilika pakubwa. Utaweza sasa kimaumbile kufaidi utambuzi katika

mambo mengi ambayo hukuyaelewa awali; bila ya kuhitaji wengine kukufunza, bila kujua, utaweza kufahamishwa na Mungu, ili uweze kuwa na fahamisho katika mambo yote na mambo yote utakayopitia yatakuwa mengi. Mungu atakuongoza wewe ili usije ukapotoka kwa vyovyote vile. Kisha utawekwa wazi kwenye njia ya kufanywa kuwa mtimilifu na Yeye.

Kukamilishwa na Mungu hakuwezi kuwa kukamilishwa kupitia kwa kula na kunywa neno la Mungu tu. Aina hii ya uzoefu inaegemea upande mmoja sana na haijumuishi pande zote; inamzuia binadamu katika uwezo mdogo sana. Kwa hiyo, binadamu hukosa chakula cha kiroho kinachohitajiwa zaidi. Kama mtapenda kukamilishwa na Mungu, lazima mjifunze kupitia mambo yote na kupatiwa nuru katika yote mnayoyapitia. Kila unapokumbwa na kitu, kiwe kizuri au kibaya, unafaa kufaidi kutoka katika kitu hicho na hakifai kukufanya ukae tu. Haijalishi ni nini, unafaa kuweza kukitilia maanani kwa kusimama upande wa Mungu, na wala si kuchambua au kukisoma kutoka kwa mtazamo wa binadamu (huku ni kupotoka katika hali unayopitia). Kama hivi ndivyo utakavyopitia mambo katika maisha yako, basi moyo wako utazidiwa na mizigo ya maisha yako; utaishi siku zote katika mwanga wa uso wa Mungu na hutaweza kupotoka kwa urahisi katika matendo yako. Binadamu wa aina hii ana matarajio makubwa. Kunazo fursa nyingi za kukamilishwa na Mungu. Yote haya yanategemea kama ni nyinyi ndinyi mnaompenda Mungu kwa kweli na kama mnalo azimio la kukamilishwa na Mungu, kupatwa na Mungu, na kupokea baraka na urithi Wake. Haitakubalika kwenu kuwa na azimio tu. Lazima muwe na maarifa mengi, vinginevyo siku zote mtapotoka katika matendo yenu. Mungu yuko radhi kumkamilisha kila mmoja wenu. Kama ilivyo sasa, ingawa wengi tayari wamekubali kazi ya Mungu kwa muda mwingi, wamejiwekea mipaka ya kufurahia tu neema ya Mungu na wako radhi tu kupokea tulizo fulani la mwili kutoka Kwake. Hawako radhi kupokea ufunuo zaidi na wa kiwango cha juu zaidi, hali ambayo inaonyesha kwamba moyo wa binadamu ungali nje siku zote. Ingawa kazi ya binadamu, huduma yake, na moyo wake wa upendo kwa Mungu vyote vina kasoro chache zaidi, kuhusiana na kiini cha binadamu na kufikiria kwake kusiko na nuru, binadamu bado daima hutafuta amani na furaha ya mwili, na huwa hajali masharti na makusudio Mungu ya katika kumkamilisha binadamu ni yapi. Kwa hivyo maisha ya wengi yangali machafu na yaliyooza, bila dalili zozote za mabadiliko. Yeye hasa haichukilii imani katika Mungu kama suala lenye umuhimu. Badala yake, ni kana kwamba anayo imani tu kwa ajili ya binadamu mwengine, akitenda bila ukweli au kujitolea, na akiishi tu kwa vile viwango vya chini zaidi vya maisha, akiendelea kuwepo tu bila kusudi lolote. Wachache ndio wanaotafuta kuingia ndani ya neno la Mungu katika mambo yote, huku wakifaidi mambo mengi ya kusitawisha, wakiwa wenye utajiri mkubwa zaidi katika nyumba ya Mungu siku hii, na wakupokea baraka zaidi za Mungu. Kama unatafuta kukamilishwa na Mungu katika mambo yote na unaweza kurithi ahadi za Mungu hapa ulimwenguni; kama unatafuta kupatiwa nuru na Mungu katika mambo yote na

huiruhusu miaka kuyoyoma tu huku ukiwa umezubaa, hii ndiyo njia inayostahili kuingia kwa bidii. Ni kupitia kwa njia hii tu ndipo unastahili na unafaa kukamilishwa na Mungu. Wewe ndiwe kweli unayetafuta kukamilishwa na Mungu? Wewe ndiwe kweli uliye mwenye bidii katika mambo yote? Unayo roho sawa ya upendo kwa Mungu kama Petro? Unayo hiari ya kumpenda Mungu kama Yesu alivyofanya? Umekuwa na imani katika Yesu kwa miaka mingi; umeona namna Yesu alivyompenda Mungu? Yesu ndiye kweli unayemwamini? Unamwamini Mungu wa matendo wa siku hii; umeona namna ambavyo Mungu wa matendo katika mwili anavyompenda Mungu kule mbinguni? Unayo imani katika Bwana Yesu Kristo; hiyo ni kwa sababu kusulubishwa kwa Yesu ili kuwakomboa wanadamu na miujiza Aliyoifanya vyote kwa ujumla ni ukweli unaokubaliwa. Hata hivyo, imani ya mwanadamu haitokani na maarifa na ufahamu wa kweli wa Yesu Kristo. Unaamini tu katika jina la Yesu lakini huna imani katika Roho Wake, kwani hujali kuhusu namna Yesu alivyompenda Mungu. Imani yako katika Mungu ni changa sana. Ingawa umekuwa na imani katika Yesu kwa miaka mingi, hujui namna ya kumpenda Mungu. Je, jambo hili halikufanyi kuwa mjinga mkubwa zaidi kote ulimwenguni? Hii inaonyesha kwamba kwa miaka mingi umekila chakula cha Bwana Yesu Kristo bure. Simpendi tu binadamu wa aina hii, Naamini kwamba pia Bwana Yesu Kristo, ambaye unamwabudu, hampendi. Mtu wa aina hii anawezaje kukamilishwa? Huaibiki? Huhisi aibu? Bado unao ujasiri wa kumkabili Bwana Yesu Kristo? Je, nyinyi nyote mnaelewa maana ya maneno Yangu?

Waovu Hakika Wataadhibiwa

Jichunguzeni ili mwone kama mnatenda haki katika kila jambo mnalotenda, na iwapo matendo yenu yote yanachunguzwa na Mungu: Hii ndiyo kanuni ambayo kwayo wale wanaomwamini Mungu wanafanya shughuli zao. Mtaitwa wenye haki kwa sababu mnaweza kumridhisha Mungu, na kwa sababu mnakubali utunzaji na ulinzi wa Mungu. Machoni pa Mungu, wote wanaokubali utunzaji, ulinzi na ukamilishaji wa Mungu, na wale wanaopatwa na Yeye, ni wenye haki, na Yeye huwaona kuwa wenye thamani. Kadri mnavyozidi kuyakubali maneno ya sasa ya Mungu, ndivyo mtakavyozidi kuweza kupokea na kuelewa mapenzi ya Mungu, na ndivyo basi mtakavyoweza kuishi kwa kudhihirisha maneno ya Mungu na kuyakidhi mahitaji Yake zaidi. Hili ndilo agizo la Mungu kwenu na ndilo jambo ambalo nyote mnapaswa kuweza kufikia. Mkitumia fikira zenu wenyewe kumpima na kumwekea Mungu mipaka, kana kwamba Mungu ni sanamu ya udongo isiyobadilika, na mkimwekea Mungu mipaka kabisa katika vigezo vya Biblia na kumweka katika mawanda ya kazi yenye mipaka, basi hii inathibitisha kwamba mmemshutumu Mungu. Kwa sababu Wayahudi katika Agano la Kale walimchukulia Mungu kuwa sanamu yenye umbo lisilobadilika waliloshikilia mioyoni mwao, kana kwamba Mungu angeweza tu kuitwa Masihi, na Yeye aliyeitwa Masihi pekee ndiye Angeweza kuwa Mungu, na kwa sababu binadamu walimtumikia na kumwabudu Mungu kana

kwamba Alikuwa sanamu ya udongo (isiyo na uhai), walimsulubisha Yesu wa wakati huo msalabani, wakimhukumu kifo—hivyo Yesu asiye na hatia Alihukumiwa kifo. Mungu hakuwa na kosa lolote, mwanadamu alikataa kumsamehe, naye alisisitiza kumhukumu afe na basi Yesu akasulubishwa. Kila wakati mwanadamu huamini kuwa Mungu habadiliki na humfafanua kwa msingi wa kitabu kimoja tu, Biblia, kana kwamba mwanadamu ana ufahamu wa kina kuhusu usimamizi wa Mungu, kana kwamba mwanadamu anavyo vitu vyote atendavyo Mungu katika kiganja cha mkono wake. Wanadamu ni wapumbavu kupita kiasi, wana kiburi kikubwa sana, na wote wana kipaji cha kutia chumvi sana wanapoelezea jambo. Bila kujali jinsi kiwango chako cha ufahamu kumhusu Mungu kilivyo, bado Nasema kwamba humfahamu Mungu, kwamba wewe ni mtu ambaye humpinga Mungu zaidi, na kwamba umemshutumu Mungu, kwa sababu huna uwezo kabisa wa kuiheshimu kazi ya Mungu na kutembea katika njia ya kufanywa kamilifu na Mungu. Kwa nini Mungu hatosheki kamwe na matendo ya mwanadamu? Kwa sababu mwanadamu hamjui Mungu, kwa sababu ana fikira nyingi sana, na kwa sababu maarifa yake kuhusu Mungu hayaafikiani na uhalisi hata kidogo, lakini badala yake hurudia tu mada ile ile bila mabadiliko na hutumia mwelekeo ule ule katika kila hali. Na hiyo, kwa kuwa Amekuja duniani leo, Mungu anasulubishwa kwa mara nyingine na mwanadamu. Wanadamu dhalimu! Kuwafumba watu macho na kula njama, kupokonyana na kunyang'anya mmoja kutoka kwa mwingine, kung'ang'ania umaarufu na mali, kuuana—haya yote yataisha lini? Licha ya mamia ya maelfu ya maneno ambayo Mungu amezungumza, hakuna hata mmoja ambaye ameacha kufanya upumbavu. Watu hutenda kwa ajili ya familia zao, watoto wao, kazi zao, matarajio yao ya baadaye, cheo, majivuno, na pesa, kwa sababu ya chakula, mavazi, na mwili. Lakini kuna yeyote ambaye matendo yake kwa kweli ni kwa ajili ya Mungu? Hata miongoni mwa wale ambao wanatenda kwa ajili ya Mungu, kunao wachache tu wanaomfahamu Mungu. Ni watu wangapi ambao hawatendi kwa ajili ya maslahi yao? Ni wangapi wasiowakandamiza na kuwatenga wengine ili kulinda vyeo vyao wenyewe? Na hivyo, Mungu amehukumiwa kifo mara nyingi kwa nguvu, na mahakimu wakatili wengi mno wamemhukumu Mungu na kumsulubisha msalabani tena. Wangapi wanaweza kuitwa wenye haki kwa sababu wanatenda mambo kwa ajili ya Mungu kwa kweli?

Je, ni rahisi sana kukamilishwa mbele ya Mungu kama mtakatifu au mtu mwenye haki? Ni kauli ya ukweli kwamba, “hakuna wenye haki katika dunia hii, wenye haki hawapo katika dunia hii.” Mnapokuja mbele za Mungu, fikirieni kile mnachovaa, tafakarini kila neno na kitendo chenu, juu ya kila fikira na wazo lenu na hata ndoto mnazoota kila siku—vyote ni kwa manufaa yenu wenyewe. Je, hivi sivyo hali halisi ilivyo? “Haki” haimaanishi kuwatolea wengine sadaka wala haimaanishi kumpenda jirani yako vile unavyojipenda na haimaanishi kuepukana na mizozo na ugomvi, au kunyang'anya na kuiba. Haki inamaanisha kuchukua agizo la Mungu

kama wajibu wako na kuiheshimu mipango na utaratibu wa Mungu kama wito wako utokao mbinguni, bila kujali wakati ama mahali, kama tu yote ambayo Bwana Yesu aliyafanya. Hii ndiyo haki ambayo amezungumzia Mungu. Kwamba Lutu aliweza kuitwa mwenye haki ni kwa sababu aliwaokoa wale malaika wawili waliotumwa na Mungu bila kuzingatia faida ama hasara yake mwenyewe; inaweza kusemwa tu kwamba alichotenda wakati huo kinaweza kuitwa haki, lakini hawezi kuitwa mwanadamu mwenye haki. Ilikuwa tu ni kwa sababu Lutu alikuwa amemwona Mungu ndipo akawatoa wasichana wake wawili badala ya malaika, lakini tabia yake yote ya hapo awali haikuwakilisha haki. Na hivyo Nasema “hakuna wenye haki katika dunia hii.” Hata kati ya wale ambao wako katika mkondo wa urejesho, hakuna hata mmoja anayeweza kuitwa mwenye haki. Haijalishi matendo yako ni mazuri vipi, haijalishi jinsi unavyoonekana kulisifu jina la Mungu, si kuwapiga na kuwalaani wengine, wala kuwaibia na kuwaporu wengine, bado huwezi kuitwa mwenye haki, kwa sababu haya ndiyo mtu wa kawaida ana uwezo wa kuwa nayo. Kilicho muhimu sasa ni kwamba wewe humfahamu Mungu. Inaweza tu kusemwa kwamba kwa sasa una kiasi kidogo cha ubinadamu wa kawaida, lakini hakuna vipengele vya haki viliyozungumziwa na Mungu, na hivyo hakuna chochote unachotenda ambacho kinaweza kuthibitisha kwamba unamfahamu Mungu.

Hapo awali, Mungu alipokuwa mbinguni, mwanadamu alimtendea Mungu kwa namna ya udanganyifu. Leo, Mungu amekuwa miongoni mwa wanadamu—hakuna anayejua imekuwa ni kwa miaka mingapi—lakini katika kufanya mambo mwanadamu bado anatenda kwa namna isiyo ya dhati na anajaribu kumdanganya Yeye. Je, mwanadamu hayuko nyuma sana katika kufikiri kwake? Ndivyo ilivyokuwa na Yuda: Kabla Yesu aje, Yuda angesema uwongo ili kuwadanganya ndugu zake, na hata baada ya Yesu kuja, bado hakubadilika; hakumjua Yesu hata kidogo, na mwishowe alimsaliti Yesu. Je, hii haikuwa kwa sababu hakumfahamu Mungu? Kama leo bado hamumfahamu Mungu, basi kuna uwezekano kwamba mnaweza kuwa Yuda mwingine, na kufuatilia hili, msiba wa kusulubiwa kwa Yesu katika Enzi ya Neema maelfu ya miaka iliyopita unaweza kurudiwa tena. Je, hamwamini hili? Ni ukweli! Hivi sasa, watu wengi wako katika hali kama hiyo—Naweza kuwa Ninayasema haya mapema sana kiasi—na watu wa aina hii wote ni wahusika wanaochukua nafasi ya Yuda. Sizungumzi upuuzi, bali kwa msingi wa ukweli—na huna budi ila kuridhika. Ingawa watu wengi wanajifanya kuwa wanyenyekevu, katika mioyo yao hakuna kingine ila dimbwi la maji yaliyokufa, handaki la maji yanayonuka. Hivi sasa kuna wengi sana wa aina hii katika kanisa na mnafikiri Sina habari yoyote kuhusu hili. Leo, Roho Wangu huniamulia na kunishuhudia. Unafikiri kwamba Sijui lolote? Je, unafikiri Sielewi lolote kuhusu fikira za ujanja katika mioyo yenu, mambo mnavyoweka katika mioyo yenu? Je, ni rahisi hivyo kumdanganya Mungu? Je, unafikiri kwamba unaweza kumtendea kwa njia yoyote unayotaka? Hapo zamani, Nilikuwa na wasiwasi msije mkazuiwa, hivyo Niliendelea kuwapa

uhuru, lakini binadamu hawakuweza kutambua kwamba Nilikuwa mzuri kwao, na Nilipowapa kidogo walitaka mengi. Ulizieni kati yenu: Sijawahi kumshughulikia yeyote, na Sijawahi kumkemea yeyote kijuujuu—na bado Sina tashwishi juu ya nia na fikira za mwanadamu. Je, unafikiri Mungu Mwenyewe, ambaye Mungu anamshuhudia, ni mjinga? Hivyo, Ninasema wewe ni kipofu sana! Sitakufunua, lakini hebu tuone tu jinsi unavyoweza kuwa mpotovu. Hebu tuone iwapo ujanja wako mdogo unaweza kukuokoa, ama iwapo kujaribu kadri uwezavyo kumpenda Mungu kutakuokoa. Leo, Sitakushutumu; hebu tungoje mpaka wakati wa Mungu tuone Atakavyokuadhibu. Sina wakati wa kupoteza kufanya maongezi madogo madogo na wewe sasa, na Sina nia ya kuchelewesha kazi Yangu kuu kwa ajili yako tu. Buu kama wewe hastahili muda utakaomchukua Mungu kukushughulikia—kwa hivyo hebu tuone tu jinsi unavyoweza kuwa mpotovu. Watu kama hawa hawafuatilii maarifa yaa Mungu hata kidogo, wala hawampendi Yeye hata kidogo, na bado wanataka Mungu awaite wenye haki—huu si utani? Kwa sababu idadi ndogo ya watu ni waaminifu kwa kweli, Nitalenga tu katika kuzidi kumpa mwanadamu uhai. Nitakamilisha tu kile Ninachohitaji kukamilisha leo, lakini katika siku zijazo Nitaleta adhabu kwa kila mmoja kulingana na kile ambacho amefanya. Nimesema yote yanayopaswa kusemwa, kwa sababu hii hasa ndiyo kazi Ninayoifanya. Ninafanya kile tu Ninachopaswa kufanya, na si kile Nisichopaswa kufanya. Hata hivyo, Natumai kwamba mtatumia muda zaidi katika kutafakari: Kiwango gani hasa cha ufahamu wako kuhusu Mungu ni cha kweli? Je, wewe ni mtu ambaye amemsulubisha Mungu kwa mara nyingine? Maneno Yangu ya mwisho ni haya: Ole wao wamsulubishao Mungu.

Jinsi ya Kuingia Katika Hali ya Kawaida

Kadiri watu wanavyokubali maneno ya Mungu zaidi, ndivyo wanavyopata nuru zaidi, na ndivyo wanavyokuwa na njaa na kiu zaidi katika kufuatilia kwao kumjua Mungu. Ni wale tu wanaoyakubali maneno ya Mungu ndio wanaoweza kuwa na uzoefu mkuu na wa kina zaidi, na wao pekee ndio ambao maisha yao yanaweza kuendelea kukua kama maua ya ufuta. Wote wanaofuatilia maisha wanapaswa kuchukulia hili kama kazi yao ya wakati wote; wanapaswa kuhisi kwamba “bila Mungu, siwezi kuishi; bila Mungu, siwezi kutimiza chochote; bila Mungu, kila kitu ni tupu.” Vile vile pia, wanapaswa kuwa na azimio kwamba “bila uwepo wa Roho Mtakatifu, sitafanya chochote, na ikiwa kuyasoma maneno ya Mungu hakuna matokeo basi sijali kufanya chochote.” Msijifurahishe. Uzoefu wa maisha hutoka kwa nuru na mwongozo wa Mungu, na ndilo dhihirisho la juhudi zenu za nafsi. Mnachopaswa kuhitaji kutoka wenyewe kufanya ni: “Inapokuja kwa suala la uzoefu wa maisha, siwezi kujipa uhuru wa kufanya nipendavyo.”

Wakati mwingine, unapokuwa katika hali zisizo zakawaida, unapoteza uwepo wa Mungu,

na unashindwa kumhisi Mungu unapoomba. Ni kawaida kuhisi hofu nyakati kama hizo. Unapaswa kuanza kutafuta mara moja. Usipofanya hivyo, Mungu atakuwa mbali zaidi na wewe, na utakuwa bila uwepo wa Roho Mtakatifu—na zaidi ya hayo, utakuwa bila kazi ya Roho Mtakatifu kwa siku moja, siku mbili, hata mwezi mmoja au miezi miwili. Katika hali hizi, unakuwa mtu asiye na hisia hata kidogo na kwa mara nyingine unachukuliwa mateka na Shetani, hadi kwa kiwango ambapo unaweza kufanya vitendo vya kila aina. Unatamani utajiri, unawadanganya ndugu zako, unatazama filamu na video, unacheza mahjong, na hata kuvuta sigara na kunywa pombe bila nidhamu. Moyo wako umepotoka mbali kutoka kwa Mungu, umeenda katika njia yako mwenyewe kwa siri, na umeihukumu kazi ya Mungu kiholela. Katika visa vingine, watu hupotoka sana kiasi kwamba hawahisi haya au aibu katika kufanya dhambi za kingono. Mtu wa aina hii ametelekezwa na Roho Mtakatifu; kwa kweli, kazi ya Roho Mtakatifu haijakuwa kwa mtu kama huyo kwa muda mrefu. Mtu anaweza tu kumwona akizama zaidi katika upotovu huku mikono ya uovu ikizidi kunyooka. Mwishowe, anakana uwepo wa njia hii, na anachukuliwa mateka na Shetani anapotenda dhambi. Ukigundua kuwa una uwepo wa Roho Mtakatifu tu, lakini huna kazi ya Roho Mtakatifu, tayari hiyo ni hali hatari kuwa ndani. Wakati huwezi hata kuhisi uwepo wa Roho Mtakatifu, basi uko karibu kufa. Usipotubu, basi utakuwa umemrudia Shetani kabisa, na utakuwa miongoni mwa wale wanaoondolewa. Kwa hivyo, unapogundua kuwa uko katika hali ambayo kuna uwepo wa Roho Mtakatifu tu (hutendi dhambi, unajizuia, na hufanyi chochote kinachompinga Mungu waziwazi) lakini unakosa kazi ya Roho Mtakatifu (huhisi kuguswa unapoomba, hupati nuru au mwangaza wa wazi unapokula na kunywa maneno ya Mungu, hujali kuhusu kula na kunywa maneno ya Mungu, hakuna ukuaji wowote katika maisha yako kamwe, na umeondolewa mwanga mkuu kwa muda mrefu sasa)—katika nyakati kama hizi, lazima uwe mwangalifu zaidi. Lazima usijifurahishe, lazima usiipe tabia yako uhuru zaidi. Uwepo wa Roho Mtakatifu unaweza kutoweka wakati wowote. Hii ndiyo maana hali kama hii ni hatari sana. Ukijipata katika hali ya aina hii, jaribu kuyabadilisha mambo haraka iwezekanavyo. Kwanza, unapaswa kusema sala ya toba na uombe kwamba Mungu akupe huruma Yake kwa mara nyingine tena. Omba kwa bidii zaidi na uutulize moyo wako ili ule na kunywa maneno zaidi ya Mungu. Ukiwa na msingi huu, lazima utumie wakati zaidi katika maombi; uongeze bidii yako mara dufu katika kuimba, kusali, kula na kunywa maneno ya Mungu, na kutekeleza wajibu wako. Unapokuwa dhaifu kabisa, moyo wako unamilikiwa na Shetani kwa urahisi kabisa. Hilo linapofanyika, moyo wako unachukuliwa kutoka kwa Mungu na kurudishwa kwa Shetani, na punde baada ya hapo unakuwa bila uwepo wa Roho Mtakatifu. Katika nyakati kama hizi, inakuwa vigumu mara dufu kupata tena kazi ya Roho Mtakatifu. Ni bora kutafuta kazi ya Roho Mtakatifu wakati bado Yeye yuko pamoja nawe, jambo ambalo litamruhusu Mungu kukupa nuru Yake zaidi na kutomfanya Akuache. Kuomba, kuimba nyimbo, kufanya shughuli yako, na kula na kunywa maneno ya Mungu—yote haya yanafanywa ili

Shetani asiwe na fursa ya kufanya kazi yake, na ili kwamba Roho Mtakatifu aweze kufanya kazi ndani yako. Usipoipata tena kazi ya Roho Mtakatifu kwa njia hii, ukingojea tu, basi kuipata tena kazi ya Roho Mtakatifu haitakuwa rahisi wakati ambapo umepoteza uwepo wa Roho Mtakatifu, isipokuwa kama Roho Mtakatifu amekugusa wewe hasa, au Amekupa nuru na kukuangazia hasa. Hata hivyo, haichukui siku moja au mbili tu kwa hali yako kurejea; wakati mwingine hata miezi sita inaweza kupita bila urejesho wowote. Hii yote ni kwa sababu watu huwa wazembe sana, hawawezi kupitia vitu kwa njia ya kawaida na hivyo wanaachwa na Roho Mtakatifu. Hata ukipata tena kazi ya Roho Mtakatifu, kazi ya sasa ya Mungu bado inaweza kukosa kuwa wazi kabisa kwako, kwa kuwa umesalia nyuma sana katika uzoefu wako wa maisha, kana kwamba umeachwa maili elfu kumi nyuma. Je, hili si jambo baya sana? Hata hivyo, nawaambia watu kama hao kwamba hawajachelewa sana kutubu sasa, lakini kwamba kuna sharti moja: Lazima ufanye kazi kwa bidii zaidi, na usijiingize katika uvivu. Ikiwa watu wengine wanaomba mara tano kwa siku moja, wewe lazima uombe mara kumi; ikiwa watu wengine wanakula na kunywa maneno ya Mungu kwa saa mbili kwa siku, wewe lazima ufanye hivyo kwa saa nne au sita; na ikiwa watu wengine wanasikiliza nyimbo kwa saa mbili, lazima wewe usikilize kwa angalau siku nusu. Kuwa na amani mara kwa mara mbele za Mungu na ufikirie kuhusu upendo wa Mungu hadi uguswe, moyo wako umrudie Mungu, na usithubutu kupotoka kutoka kwa Mungu—ni hapo tu ndipo matendo yako yatazaa matunda; ni hapo tu ndipo utaweza kurejesha hali yako ya kawaida ya zamani.

Watu wengine huweka shauku nyingi katika ufuatiliaji wao na bado hushindwa kuingia kwenye njia sahihi. Hii ni kwa sababu wao ni wazembe sana na hawatilii maanani mambo ya kiroho. Hawajui jinsi ya kupitia maneno ya Mungu, na hawajui kazi na uwepo wa Roho Mtakatifu ni nini. Watu kama hawa ni wenye shauku lakini ni wapumbavu; hawafuatilii uzima. Hiyo ni kwa sababu huna maarifa hata kidogo ya Roho, hujui chochote kuhusu ukuaji katika kazi inayoendelea ya Roho Mtakatifu, na hujui kuhusu hali iliyo ndani ya roho yako mwenyewe. Je, imani ya watu kama hao siyo aina ya imani iliyo pumbavu? Ufuatiliaji wa watu kama hao hatimaye hauzai chochote. Jambo la muhimu katika kufikia ukuaji wa maisha katika imani ya mtu kwa Mungu ni kujua ni kazi gani ambayo Mungu hufanya katika uzoefu wako, kuona uzuri wa Mungu, na kuelewa mapenzi ya Mungu, kiasi kwamba unastahi mipango yote ya Mungu, maneno ya Mungu yanakita mizizi ndani yako ili yawe uzima wako, na hivyo kumridhisha Mungu. Ikiwa imani yako ni imani ya kipumbavu, ikiwa hutilii maanani mambo ya kiroho na mabadiliko katika tabia yako ya maisha, ikiwa huweki jitihada yoyote kwa ukweli, je, utaweza kuyaelewa mapenzi ya Mungu? Ikiwa huelewi kile ambacho Mungu anataka, basi hutaweza kupata uzoefu, na hivyo hutakuwa na njia ya kutenda. Kile ambacho lazima uzingatie unapopitia maneno ya Mungu ni matokeo ambayo maneno hayo yanatoa ndani yako, ili uweze kumjua

Mungu kutoka katika maneno Yake. Ikiwa wewe unajua tu jinsi ya kusoma maneno ya Mungu, lakini hujui jinsi ya kuyapitia, je, hili halionyeshi kuwa wewe hujui kuhusu mambo ya kiroho? Hivi sasa, watu wengi hawawezi kuyapitia maneno ya Mungu, na hivyo hawajui kazi ya Mungu. Je, huku si kushindwa katika kutenda kwao? Wakiendelea kwa namna hii, ni lini wataweza kupitia mambo kwa uzuri wake mkamilifu na kufanikisha ukuaji katika maisha yao? Je, haya si mazungumzo matupu tu? Kuna wengi kati yenu wanaozingatia nadharia, ambao hawajui chochote kuhusu masuala ya kiroho, na bado wanatamani kutumiwa sana na Mungu na kubarikiwa na Mungu. Hili ni jambo lisilowezekana kabisa! Kwa hivyo, lazima mkomeshe kushindwa huku, ili nyote muweze kuingia kwenye njia sahihi katika maisha yenu ya kiroho, muwe na uzoefu halisi, na muingie katika uhalisi wa maneno ya Mungu kwa kweli.

Jinsi ya Kuhudumu kwa Upatanifu na Mapenzi ya Mungu

Mtu anapomwamini Mungu, mtu anapaswa kumtumikiaje, hasa? Ni masharti yapi yanayopaswa kutimizwa na ni ukweli upi unaopaswa kufahamika na wale wanaomhudumia Mungu? Na ni wapi unapoweza kuwa ukikengeuka katika huduma yako? Unapaswa kuwa na majibu ya mambo haya yote. Masuala haya yanagusia jinsi unavyomwamini Mungu, jinsi unavyotembea katika njia ya kuongozwa na Roho Mtakatifu, na jinsi unatii mipango ya Mungu katika mambo yote, na yatakuwezesha kujua kila hatua ya kazi ya Mungu ndani yako. Ukifika mahali hapo utafurahia kujua imani katika Mungu ni nini, namna ya kumwamini Mungu vizuri, na kile unachopaswa kufanya ili kutenda mambo kwa upatanifu na mapenzi ya Mungu. Hili litakufanya utii kikamilifu kazi ya Mungu, na hutakuwa na malalamiko, hutahukumu, au kuchambua, sembuse kutafiti. Zaidi ya hayo, nyote mtakuwa na uwezo wa kumtii Mungu hadi kifo, mkimruhusu Mungu awaongoze na kuwachinja kama kondoo, ili nyote muweze kuwa akina Petro wa miaka ya tisini, na muweze kumpenda Mungu kwa hali ya juu sana hata msalabani, bila malalamiko yoyote. Hivyo ndivyo mtakavyoweza kuishi kama akina Petro wa miaka ya tisini.

Kila mtu ambaye ameamua anaweza kumhudumia Mungu—lakini ni lazima iwe kwamba wale tu ambao wanayashughulikia kwa makini mapenzi ya Mungu na kuyafahamu mapenzi ya Mungu ndio wanaohitimu na walio na haki ya kumhudumia Mungu. Nimegundua hili kati yenu: Watu wengi wanaamini ya kuwa bora tu wanaeneza injili kwa bidii kwa ajili ya Mungu, waende barabarani kwa ajili ya Mungu, wajitumie na kuacha vitu kwa ajili ya Mungu, na kadhalika, basi huku ni kumhudumia Mungu; hata zaidi, watu wa kidini huamini kwamba kumhudumia Mungu kuna maana ya kukimbia hapa na pale wakiwa na Biblia mikononi mwao, wakieneza injili ya ufalme wa mbinguni na kuwaokoa watu kwa kuwafanya watubu na kuungama; kuna wakuu wengi wa kidini wanaofikiri kwamba kumhudumia Mungu ni kuhubiri makanisani baada ya kusoma na kufunzwa katika chuo cha seminari, kuwafunza watu kwa kusoma sura za Biblia; pia

kuna watu katika maeneo ya umaskini wanaoamini kwamba kumhudumia Mungu kuna maana ya kupokea uponyaji na kufukuza mapepo, au kuwaombea ndugu, au kuwahudumia; miongoni mweni, kuna wengi wanaoamini kwamba kumhudumia Mungu kuna maana ya kula na kunywa maneno ya Mungu, kumwomba Mungu kila siku, na pia kutembelea na kufanya kazi katika makanisa kila mahali; kuna ndugu wengine wanaoamini kwamba kumhudumia Mungu kunamaanisha kutoolewa wala kulea familia kamwe, na kutoa nafsi zao zote kwa Mungu. Ilhali watu wachache wanajua maana ya kweli ya kumhudumia Mungu. Ingawa kuna wengi wanaomhudumia Mungu kama nyota angani, idadi ya wale wanaoweza kuhudumu moja kwa moja, na wanaoweza kutumikia kulingana na mapenzi ya Mungu, ni hafifu—ndogo isiyo na maana. Kwa nini Ninasema hivi? Ninasema hivi kwa sababu wewe hufahamu kiini cha fungu la maneno “huduma kwa Mungu,” na unafahamu machache sana kuhusu jinsi ya kutumikia kulingana na mapenzi ya Mungu. Kuna hitaji la haraka kwa watu kuelewa hasa ni aina gani ya huduma kwa Mungu ndiyo inayoweza kulingana na mapenzi Yake.

Ikiwa ungependa kutumikia kulingana na mapenzi ya Mungu, ni lazima kwanza ufahamu ni watu wa aina gani wanamfurahisha Mungu, ni watu wa aina gani wanachukiwa na Mungu, ni watu wa aina gani wanafanywa kuwa kamili na Mungu, na ni watu wa aina gani wana sifa zinazostahili kumhudumia Mungu. Hiki ni kiasi kidogo zaidi unachopaswa kujiandaa nacho. Isitoshe, unapaswa kujua malengo ya kazi ya Mungu, na kazi ambayo Mungu Ataitenda hapa na wakati huu. Baada ya kufahamu haya, na kupitia kwa mwongozo wa maneno ya Mungu, kwanza unafaa kuingia, na kupokea agizo la Mungu kwanza. Unapopata uzoefu wa kweli kwa msingi wa maneno ya Mungu, na unapojua kweli kazi ya Mungu, utakuwa umehitimu kumhudumia Mungu. Na unapomhudumia ndipo Mungu hufungua macho yako ya kiroho, na kukuruhusu kuwa na ufahamu mkubwa zaidi wa kazi Yake na kuiona dhahiri zaidi. Ukiingia katika ukweli huu, uzoefu wako utakuwa wa kina zaidi na wa kweli, na wale wote ambao wamepata uzoefu wa aina hiyo wataweza kutembea miongoni mwa makanisa mengi na kuwatolea ndugu zako, ili muweze kutumia nguvu za kila mmoja kufidia upungufu wako na kupata maarifa mengi zaidi ndani ya roho zenu. Ni baada tu ya kutimiza matokeo haya ndipo utakapoweza kutumikia kulingana na mapenzi ya Mungu na kufanywa mkamilifu na Mungu wakati wa kufanya huduma yako.

Wanaomhudumia Mungu wanapaswa kuwa marafiki wema wa Mungu, wanapaswa kumfurahisha Mungu, na kuwa na uaminifu wa hali ya juu kwa Mungu. Bila kujali iwapo unatenda bila kuonekana na watu, au mbele ya watu, unaweza kupata furaha ya Mungu mbele za Mungu, unaweza kusimama imara mbele za Mungu, na bila kujali jinsi watu wengine wanavyokutendea, wewe huifuata njia yako mwenyewe kila mara, na kuushughulikia kwa makini mzigo wa Mungu. Mtu wa aina hii pekee ndiye rafiki mwema wa Mungu. Marafiki wema wa Mungu wanaweza kumhudumia Yeye moja kwa moja kwa sababu wamepewa agizo kuu la

Mungu, na mzigo wa Mungu, wao wanaweza kuuchukulia moyo wa Mungu kama moyo wao wenyewe, na mzigo wa Mungu kama mzigo wao wenyewe, na hawazingatii iwapo watafaidi au watapoteza matarajio: Hata wasipokuwa na matarajio, na hawatafaidi chochote, watamwamini Mungu daima kwa moyo wa upendo. Kwa hivyo, mtu wa aina hii ni rafiki mwema wa Mungu. Marafiki wema wa Mungu ni wasiri Wake pia; ni wasiri wa Mungu pekee ndio wanaoweza kushiriki katika kutotulia Kwake, matamania Yake, na ingawa mwili wao una uchungu na ni mdhaifu, wanaweza kuvumilia uchungu na kuacha kile wanachokipenda ili kumridhisha Mungu. Mungu huwapa watu wa aina hii mizigo mingi, na kile ambacho Mungu anataka kufanya kinathibitishwa katika ushuhuda wa watu kama hawa. Yaani, watu hawa wanapendwa na Mungu, wao ni watumishi wa Mungu wanaoupendeza moyo Wake, na ni watu wa aina hii pekee ndio wanaoweza kutawala pamoja na Mungu. Ukishakuwa rafiki mwema wa Mungu ndipo utakapoweza kabisa kutawala pamoja na Mungu.

Yesu aliweza kukamilisha agizo la Mungu—kazi ya ukombozi wa wanadamu wote—kwa sababu alikabidhi kila tatizo kwa mapenzi ya Mungu, bila kufuata mipango na fikira Zake binafsi. Basi pia, Yeye Alikuwa rafiki mwema wa Mungu—Mungu Mwenyewe, jambo ambalo nyote mnalielewa vizuri sana. (Kwa kweli, alikuwa Mungu Mwenyewe aliyetolewa ushahidi na Mungu; Ninataja jambo hili hapa kwa kuutumia ukweli wa Yesu ili kuonyesha mfano wa suala hili.) Aliweza kuuweka mpango wa usimamizi wa Mungu katika kiini cha mambo yote, na kila mara alimwomba Baba wa mbinguni na kuyatafuta mapenzi ya Baba wa mbinguni. Aliomba, na kusema: “Mungu Baba! Timiza kile ambacho ni mapenzi Yako, na usitende kulingana na nia Zangu; ingekuwa heri ukitenda kulingana na mpango Wako. Mwanadamu anaweza kuwa dhaifu, lakini kwa nini unapaswa kumshughulikia? Ni vipi ambavyo mwanadamu anaweza kustahili kukuhangaisha, mwanadamu ambaye ni kama chungu mkononi Mwako? Ndani ya moyo Wangu, Ninatamani tu kutimiza mapenzi Yako, na Ninatamani Utende Unachotaka kutenda ndani Yangu kulingana na makusudio Yako mwenyewe.” Alipokuwa njiani kuelekea Yerusalemu, Yesu alihisi maumivu makali, kama kwamba kisu kilikuwa kimedungwa ndani ya moyo Wake, ilhali hakuwa na nia yoyote ya kwenda kinyume cha Neno lake; kila mara kulikuwa na nguvu zenye uwezo mkuu zilizomvutia Yeye kuelekea mahali ambapo Angesulubiwa. Mwishowe, alipigiliwa misumari juu ya msalaba na akawa mfano wa mwili wenye dhambi, akiikamilisha kazi hiyo ya ukombozi wa wanadamu, na kufufuka kutoka kwa pingu za kifo na Kuzimu. Mbele Yake, kifo, jehanamu, na Kuzimu vilipoteza nguvu zao, na vilishindwa Naye. Aliishi miaka thelathini na tatu, na katika miaka hiyo yote daima Alifanya kila Alichoweza kutimiza mapenzi ya Mungu kulingana na kazi ya Mungu wakati huo, bila kuzingatia atakachofaidi au kupoteza Yeye binafsi, na kila mara akiwaza kuhusu mapenzi ya Mungu Baba. Hivyo, baada ya Yeye kubatizwa, Mungu alisema: “Huyu ni Mwana wangu Mpendwa, ambaye Ninapendezwa naye.” Kwa sababu

ya huduma Yake mbele ya Mungu, iliyokuwa na upatanifu na mapenzi ya Mungu, Mungu aliweka mzigo mzito wa kuwakomboa wanadamu wote juu ya mabega yake na akamfanya ajitolee kuutimiza, na Alikuwa na ujuzi na ustahiki wa kuikamilisha kazi hii muhimu. Katika maisha Yake yote, alivumilia mateso yasiyokuwa na kipimo kwa ajili ya Mungu, na alijaribiwa na Shetani mara nyingi, lakini hakufa moyo. Mungu alimpa kazi ya aina hiyo kwa sababu Alimwamini Yeye, na kumpenda Yeye, na hivyo basi Mungu mwenyewe alisema: “Huyu ni Mwana wangu Mpendwa, ambaye Ninapendezwa naye.” Wakati huo, ni Yesu pekee ambaye angeweza kutimiza agizo hili, na hii ilikuwa sehemu moja ya Mungu kutimiza kazi Yake ya kuwakomboa wanadamu wote katika Enzi ya Neema.

Ikiwa, kama Yesu, unaweza kuushughulikia kwa makini mzigo wa Mungu, na kuyakataa mambo ya mwili wako, Mungu atakuaminia kazi Zake muhimu, ili uweze kufikia masharti ya kumhudumia Mungu. Ni katika hali hizo pekee ndipo utakapothubutu kusema kwamba unafanya mapenzi ya Mungu na kukamilisha agizo Lake, hapo ndipo utakapothubutu kusema unamhudumia Mungu kweli. Ukilinganishwa na mfano wa Yesu, unaweza kuthubutu kusema kwamba wewe ni mwandani wa Mungu? Je, unaweza kuthubutu kusema kwamba unafanya mapenzi ya Mungu? Je, unaweza kuthubutu kusema kwamba kweli unamhudumia Mungu? Leo, hufahamu aina hii ya huduma kwa Mungu, unaweza kuthubutu kusema kwamba wewe ni rafiki mwema wa Mungu? Ukisema kwamba unamhudumia Mungu, humkufuru Yeye? Fikiria kuhusu hilo: Je, unamhudumia Mungu, au unajihudumia wewe mwenyewe? Unamhudumia Shetani, ilhali kwa ukaidi unasema kwamba unamhudumia Mungu—katika jambo hili humkufuru Mungu? Watu wengi walio nyuma Yangu wanatamani baraka ya cheo, wana ulafi wa chakula, wanapenda kulala na kuushughulikia mwili kwa makini, kila mara wakiogopa kwamba hakuna njia ya kuondoka ndani ya mwili. Hawaifanyi kazi yao ya kawaida kanisani, lakini wanalitumia kanisa vibaya, au wanawaonya ndugu zao kwa maneno Yangu, wanasimama juu na kuwatawala wengine. Watu hawa huendelea kusema kwamba wanafanya mapenzi ya Mungu, wao husema kila mara kwamba ni marafiki wema wa Mungu—huu si upuuzi? Ikiwa una motisha iliyo sahihi, lakini huwezi kutumikia kulingana na mapenzi ya Mungu, basi wewe unakuwa mpumbavu; lakini ikiwa motisha yako si sahihi, na bado unasema kwamba unamhudumia Mungu, basi wewe ni mtu anayempinga Mungu, na unastahili kuadhibiwa na Mungu! Sina huruma kwa watu wa aina hiyo! Wao ni doezi katika nyumba ya Mungu, na kila mara wao hutamani raha za mwili, na hawazingatii mambo ambayo Mungu anayapenda; kila mara wao hutafuta mambo yaliyo mazuri kwao, wala hawatilii maanani mapenzi ya Mungu, mambo yote wanayoyafanya hayaongozwi na Roho wa Mungu, kila mara wao hufanya hila dhidi ya ndugu zao na kuwadanganya, na kuwa ndumakuwili, kama mbweha ndani ya shamba la mizabibu, akiiba mizabibu kila mara na kulikanyaga na kuliharibu shamba la mizabibu. Je, watu wa aina hiyo wanaweza kuwa marafiki

wema wa Mungu? Je, unastahili kupokea baraka za Mungu? Wewe huwajibiki kuhusu maisha yako na kanisa, unastahili kupokea agizo la Mungu? Ni nani anayeweza kuthubutu kumwamini mtu kama wewe? Unapohudumu kwa njia hii, je, Mungu anaweza kuthubutu kukuaminia kazi kubwa zaidi? Je, si wewe unachelewesha mambo?

Nasema hivi ili uweze kujua masharti yanayohitajika kutimizwa ili kuhudumu kwa upatanifu na mapenzi ya Mungu. Usipoutoa moyo wako kwa Mungu, usipoyashughulikia kwa makini mapenzi ya Mungu kama alivyofanya Yesu, basi huwezi kuaminiwa na Mungu, na mwishowe utahukumiwa na Mungu. Labda leo, katika huduma yako kwa Mungu, kila mara wewe huficha kusudi la kumdanganya Mungu na kila mara wewe humtendea kwa njia isiyo ya dhati. Kwa ufupi, bila kujali chochote kingine, ukimdanganya Mungu, hukumu isiyo ya huruma itakujia. Unapaswa kutumia vizuri nafasi ya kuwa umeingia katika njia sahihi ya kumhudumia Mungu kwa kumpa Mungu moyo wako kwanza, bila kugawanya uaminifu wako. Bila kujali iwapo uko mbele za Mungu, au mbele ya watu wengine, moyo wako unapaswa kuelekezwa kwa Mungu kila wakati, na unapaswa kufanya uamuzi wa kumpenda Mungu kama Yesu. Kwa kufanya hivi, Mungu atakufanya uwe mkamilifu, ili uwe mtumishi wa Mungu anayempendeza Mungu. Ikiwa ungependa kweli kufanywa mkamilifu na Mungu, na huduma yako iwe katika upatanifu na mapenzi Yake, basi unapaswa kubadilisha maoni yako ya awali kuhusu imani kwa Mungu, na kubadilisha jinsi ulivyokuwa ukimhudumia Mungu, ili nafsi yako yote iweze kufanywa kuwa kamilifu na Mungu; kwa kufanya hivi, Mungu hatakuacha, na, kama Petro, utakuwa katika kikosi cha mbele cha wale wanaompenda Mungu. Ukibaki kuwa mtu asiyetubu, basi utakutana na mwisho kama wa Yuda. Hii inapaswa kufahamika na watu wote wanaomwamini Mungu.

Jinsi ya Kujua Uhalisi

Mungu ni Mungu wa uhalisi: kazi Zake zote ni halisi, maneno yote Anayoyanena ni halisi, na ukweli wote Anaouonyesha ni halisi. Kila kisicho maneno Yake ni kitupu, kisichokuwepo, na kisicho timamu. Leo, Roho Mtakatifu yupo kwa ajili ya kuwaongoza watu katika maneno ya Mungu. Ikiwa watu wanatafuta kuingia katika uhalisi, basi ni lazima wauandame uhalisi, na waujue uhalisi, baadaye ni lazima wapitie uhalisi, na kuishi kwa kudhihirisha uhalisi. Kadiri watu wanavyojua uhalisi zaidi, kadiri wanavyoweza kugundua ikiwa maneno ya wengine ni halisi; kadiri watu wanavyojua uhalisi zaidi, ndivyo wanavyokuwa na dhana chache zaidi; kadiri watu wanavyopitia uhalisi zaidi, kadiri wanavyojua zaidi matendo ya Mungu wa uhalisi, na ndivyo inavyokuwa rahisi kwao kujiweka huru kutokana na tabia zao potovu na za kishetani; kadiri watu walivyo na uhalisi mkubwa, ndivyo wanavyomjua Mungu zaidi na kuuchukia mwili zaidi na kupenda ukweli; na kadiri watu walivyo na uhalisi mkubwa, ndivyo wanavyofika karibu

na ubora wa mahitaji ya Mungu. Watu waliopatikana na Mungu ni wale walio na uhalisi, na wanaojua uhalisi; wale ambao wamepatikana na Mungu wamepata kuyajua matendo halisi ya Mungu kutokana na kupitia katika uhalisi. Kadiri hasa unavyoshirikiana zaidi na Mungu na kuudhibiti mwili wako, ndivyo utakavyopokea zaidi kazi ya Roho Mtakatifu, ndivyo utakavyopata uhalisi zaidi, na ndivyo utapatiwa nuru zaidi na Mungu—na hivyo ukubwa wa ufahamu wako wa matendo halisi ya Mungu. Ikiwa unaweza kuishi katika mwangaza wa sasa wa Roho Mtakatifu, njia ya sasa ya kutenda itakuwa wazi kwako, na utaweza kujitenga zaidi na dhana za kidini na vitendo vilivyopita zamani. Leo tunalenga uhalisi: Kadiri watu walivyo na uhalisi zaidi, ndivyo ufahamu wao wa ukweli unavyokuwa wazi, na ufahamu wao wa mapenzi ya Mungu unaongezeka. Uhalisi unaweza kuzishinda nyaraka zote na mafundisho yote ya kidini, unaweza kushinda nadharia na utaalamu wote, na kadiri watu wanavyoangazia uhalisi zaidi, ndivyo wanavyompenda Mungu kwa dhati zaidi na kuyatamani maneno Yake. Ikiwa daima unalenga uhalisi, falsafa yako ya maisha, dhana za kidini, na tabia asilia zitafutwa kutokana na kazi ya Mungu. Wale wasiouandama uhalisi, na hawafahamu uhalisi, wanaelekea kutafuta kile kilicho na nguvu za juu, na watalaghaiwa kwa urahisi. Roho Mtakatifu hana namna ya kufanya kazi ndani ya watu kama hao, na kwa hivyo wanajisikia watupu, na kwamba maisha yao hayana maana.

Roho Mtakatifu anaweza tu kufanya kazi ndani yako ukijifunza kweli, ukitafuta kweli, ukiomba kweli, na ukiwa radhi kuteseka kwa ajili ya kuutafuta ukweli. Wale ambao hawautafuti ukweli hawana chochote ila tu nyaraka na mafundisho ya kidini, na nadharia tupu, na wale wasio na ukweli kiasili wana dhana nyingi kuhusu Mungu. Watu kama hawa hutamani tu Mungu aibadilishe miili yao ya nyama kuwa miili ya kiroho ili kwamba waweze kupaa katika mbingu ya tatu. Hawa watu ni wapumbavu kiasi gani? Wote wasemao mambo sampuli hii hawana ufahamu wa Mungu, au uhalisi; watu kama hawa hawawezi kushirikiana na Mungu, na wanaweza tu kusubiri bila kufanya chochote. Ikiwa watu wanataka kuelewa ukweli, na kuuona ukweli wazi wazi, na ikiwa, aidha, wanataka kuingia ndani ya ukweli, na kuuweka katika vitendo, ni sharti wajifunze kweli, watafute kweli, na wawe na hitaji la kweli. Unapotamani, na unaposhirikiana na Mungu kweli, Roho wa Mungu kwa hakika atakugusa na kufanya kazi ndani yako, jambo ambalo litakuletea nuru zaidi na kukupa ufahamu zaidi kuhusu uhalisi na kuwa wa msaada mkubwa kwa maisha yako.

Ikiwa watu wanataka kumjua Mungu, ni sharti kwanza wajue kuwa Mungu ni Mungu halisi, na ni sharti wajue maneno ya Mungu, kuonekena halisi kwa Mungu katika mwili, kazi halisi ya Mungu. Ni baada tu ya kujua kwamba kazi ya Mungu ni halisi ndiyo utaweza kweli kushirikiana na Mungu, na ni kupitia kwa njia hii tu ndipo utaweza kutimiza ukuaji wa maisha yako. Wale wote wasiokuwa na ufahamu wa uhalisi hawana namna ya kuyapitia maneno ya Mungu,

wametekwa katika dhana zao, wanaishi katika mawazo yao, na hivyo hawana ufahamu wa maneno ya Mungu. Kadiri ufahamu wako kuhusu uhalisi ulivyo mkubwa, ndivyo unakuwa karibu zaidi na Mungu, na ndivyo unakuwa rafiki Yake wa karibu zaidi; jinsi unavyotafuta zaidi kutokuwa yakini na udhahania, na mafundisho ya kidini, ndivyo unavyojitenga zaidi na Mungu, na ndivyo utakavyohisi zaidi kuwa kuyapitia maneno ya Mungu ni kazi na ni kugumu, na kwamba huna uwezo wa kuingia. Ikiwa unataka kuingia katika uhalisi wa maneno ya Mungu, na katika njia sahihi ya maisha yako ya kiroho, ni sharti kwanza ujue uhalisi na ujitenge na vitu visivyo yakini na vya miujiza—ambako ni kumaanisha kuwa, kwanza ni sharti uelewe jinsi Roho Mtakatifu anapeana nuru na kukuongoza kutoka ndani. Kwa njia hii, ikiwa kwa kweli unaweza kuelewa kazi ya Roho Mtakatifu ndani yako, utakuwa umeingia katika njia sahihi ya kufanywa mkamilifu na Mungu.

Leo, kila kitu kinaanza kwa uhalisi. Kazi ya Mungu ndiyo halisi zaidi, na inaweza kuguswa na watu; ndicho kitu kinachoweza kupitiwa na wanadamu, na kufanikisha. Ndani ya watu mna mengi ambayo si yakini na ya miujiza, ambayo yanawazuia kuijua kazi ya sasa ya Mungu. Hivyo katika mazoea yao mara zote hupotoka na kuhisi vigumu, ambayo yote yanasababishwa na dhana zao. Watu wanashindwa kuelewa kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu, hawajui uhalisi, na kwa hivyo daima njia zao za kuingia ni hasi. Wanatazama mahitaji ya Mungu kwa mbali, bila kuweza kuyatimiza; wanaona tu kwamba maneno ya Mungu kwa hakika ni mazuri, ila hawawezi kupata njia ya kuingilia. Roho Mtakatifu anafanya kazi kwa kanuni hii: kupitia ushirikiano na watu, kupitia kwa wao kuomba kimatendo, kumtafuta na kusonga karibu na Mungu, matokeo yanaweza kupatikana na wanaweza kupata nuru na kuangaziwa na Roho Mtakatifu. Si kwamba Roho Mtakatifu anafanya kazi kivyake, au mwanadamu anafanya kazi kivyake. Wote ni wa muhimu, na jinsi wanadamu wanavyoshiriki zaidi na jinsi wanavyotaka zaidi kufikia viwango vya mahitaji ya Mungu, ndivyo kazi ya Roho Mtakatifu inaimarika. Ni ushirikiano halisi tu wa wanadamu, kupitia kazi ya Roho Mtakatifu, ndivyo vinaweza kutoa matukio halisi na ufahamu wa kweli wa kazi ya Mungu. Hatua kwa hatua, kupitia kwa mazoea kwa njia hii, mwanadamu mkamilifu hatimaye huzalishwa. Mungu hafanyi vitu vya miujiza; katika dhana za mwanadamu, Mungu ni mwenye uweza, na kila kitu kinafanywa na Mungu—na hutokea kwamba watu wanasubiri tu bila kufanya chochote, hawasomi maneno ya Mungu au kuomba, na wanasubiri tu kuguswa na Roho Mtakatifu. Walio na ufahamu sahihi, hata hivyo, wanaamini hili: matendo ya Mungu yanaweza kufikia pale ambapo ushirikiano wangu umefikia, na athari ya kazi ya Mungu kwangu inategemea namna ninavyoshirikiana. Mungu anenapo, ninapaswa kufanya lolote niwezalo na kuyaelekea maneno ya Mungu; hili ndilo ninapaswa kufanikisha.

Kati ya Petro na Paulo, mnaweza kuona wazi kuwa Petro ndiye alikuwa makini kwa uhalisi. Kutokana na yale aliyoyapitia Petro, inaweza kuonekana kuwa matukio aliyopitia yalijumlisha

mafunzo kutoka kwa wale walioanguka awali, na kwamba alipokea nguvu za watakatifu wa zamani—na kutokana na hili inaonekana hasa jinsi matukio aliyopitia Petro yalivyokuwa, kwamba yalitoshwa kuwapa watu fursa ya kuyagusa, na kuwa na uwezo wake, na kwamba yalitimizwa na watu. Paulo, ijapokuwa alikuwa tofauti: yale aliyonena kuhusu hayakuwa yakini na hayakuonekana, mambo kama kwenda katika mbingu ya tatu, kupanda katika kiti cha ufalme, na taji la wenye haki. Aliangazia masuala ya nje: kuhusu hadhi, na kuwakemea watu, na kujivunia ukuu wake, kuguswa na Roho Mtakatifu, na kadhalika. Hakuna lililokuwa halisi miongoni mwa mambo aliyoyatafuta, na mengi yake yalikuwa ndoto, na kwa hivyo inaweza kuonekana kwamba yote ambayo ni miujiza, kwa mfano ni mara ngapi Roho Mtakatifu anawagusa watu, furaha kubwa ambayo watu wanafurahia, kwenda katika mbingu ya tatu, au mafunzo ya mara kwa mara na kuyafurahia kwa kiwango fulani, kusoma maneno ya Mungu na kuyafurahia kwa kiwango fulani—hakuna lililo halisi miongoni mwa haya. Kazi yote ya Roho Mtakatifu ni ya kawaida, na halisi. Usomapo maneno ya Mungu na kuomba, ndani unang’aa na kuwa imara, dunia ya nje haiwezi kuhitilafiana na wewe, ndani unakuwa radhi kumpenda Mungu, uko radhi kushughulika na mambo chanya, na unachukia dunia potovu; huku ni kuishi ndani ya Mungu. Si kama watu wasemavyo, kufurahia kupindukia—maneno kama hayo si halisi. Leo, kila kitu kinapaswa kuanzia kwa uhalisi. Kila kitu ambacho Mungu anafanya ni halisi, na katika matukio unayoyapitia, unapaswa kuwa makini kumjua Mungu kweli, na kuzitafuta nyayo za kazi ya Mungu na namna ambazo Roho Mtakatifu anawagusa na kuwapa watu nuru. Ikiwa unakula na kunywa maneno ya Mungu, na kuomba, na kushirikiana kwa njia iliyo halisi zaidi, kuchukua kilichokuwa kizuri zama zilizopita, na kukataa kilichokuwa kibaya kama Petro, ukisikiliza na masikio yako na kuangalia na macho yako, na kuomba mara kwa mara na kutafakari moyoni mwako, na kufanya lolote uwezalo kushirikiana na kazi ya Mungu, basi kwa hakika Mungu atakuongoza.

Kuhusu Maisha ya Kawaida ya Kiroho

Imani katika Mungu husababisha maisha ya kawaida ya kiroho, ambayo ndiyo msingi wa kupitia maneno ya Mungu na kuingia katika uhalisi. Je, matendo yenu yote ya sasa ya maombi, ya kumkaribia Mungu, ya kuimba nyimbo za dini, sifa, taamali na kutafakari maneno ya Mungu yanajumuisha “maisha ya kawaida ya kiroho”? Hakuna mmoja kati yenu anayeonekana kujua. Maisha ya kawaida ya kiroho hayazuiliwi katika matendo kama kuomba, kuimba nyimbo za kidini, kushiriki katika maisha ya kanisa, na kula na kunywa maneno ya Mungu. Badala yake, yanahusisha kuishi maisha mapya na machangamfu ya kiroho. Kilicho muhimu si jinsi unavyotenda, lakini matunda yanayozalishwa na kutenda kwako. Watu wengi sana huamini kwamba maisha ya kawaida ya kiroho ni lazima yahusishe kuomba, kuimba nyimbo za kidini, kula na kunywa maneno ya Mungu ama kutafakari maneno Yake, bila kujali iwapo matendo

kama haya kweli yana athari yoyote ama yanasababisha ufahamu wa kweli. Watu hawa hulenga kufuata taratibu za kijuujuu bila kufikiria matokeo yake, wao ni watu wanaoishi katika kaida za kidini, sio watu wanaoishi ndani ya kanisa, sembuse watu wa ufalme. Maombi yao, kuimba nyimbo za kidini, na kula na kunywa maneno ya Mungu ni kufuata kanuni tu, vitu vinavyofanywa kwa sababu ya kulazimishwa na kuwa sambamba na mitindo, sio kwa sababu ya kutaka wala kutoka moyoni. Bila kujali jinsi watu hawa wanavyoomba ama kuimba, juhudi zao hazitazaa matunda, kwa kuwa kile wanachotenda ni kanuni na kaida za kidini tu; kwa kweli hawatendi maneno ya Mungu. Wanalenga tu kulalamika kuhusu jinsi ya kutenda, na wanayachukulia maneno ya Mungu kama kanuni za kufuatwa. Watu kama hawa hawatii maneno ya Mungu katika vitendo; wanaridhisha tu mwili, na kutenda ili watu wengine wawaone. Kanuni na kaida hizi za kidini zote zina asili yake kwa binadamu; hazitoki kwa Mungu. Mungu hafuati sheria, wala Haathiriwi na sheria yoyote. Badala yake, Yeye hufanya mambo mapya kila siku, Akitimiza kazi ya vitendo. Kama watu katika Kanisa la Kanuni Tatu za Binafsi, wanaojiwekea mipaka kwa matendo kama vile kuhudhuria ibada za asubuhi kila siku, kutoa sala za jioni na sala za shukrani kabla ya milo, na kutoa shukrani katika vitu vyote—bila kujali kiasi wanachofanya ama wanakifanya kwa muda gani, hawatakuwa na kazi ya Roho Mtakatifu. Watu wanapoishi kati ya kanuni na kuzingatia mbinu za utendaji, Roho Mtakatifu hawezi kufanya kazi, kwa sababu mioyo yao imejazwa na kanuni na fikira za kibinadamu. Kwa hivyo, Mungu hawezi kuingilia kati na kuwafanyia kazi, na wanaweza tu kuendelea kuishi wakidhibitiwa na sheria. Watu kama hawa daima hawawezi kupokea sifa ya Mungu.

Maisha ya kawaida ya kiroho ni maisha ambayo mtu anaishi mbele za Mungu. Mtu anapoomba, anaweza kuutuliza moyo wake mbele za Mungu, na kupitia maombi, mtu anaweza kutafuta nuru ya Roho Mtakatifu, ayajue maneno ya Mungu na aelewe mapenzi ya Mungu. Kwa kula na kunywa maneno Yake, watu wanaweza kupata ufahamu dhahiri na kamili zaidi wa kazi ya sasa ya Mungu. Pia wanaweza kupata njia mpya ya kutenda, na hawatashikilia ile ya kale; yote wanayotenda yatakuwa ili kufanikisha ukuaji katika maisha. Kuhusiana na maombi, hayahusu kunena maneno machache yanayosikika kuwa mazuri ama kulia kwa ghafla mbele za Mungu ili kuonyesha jinsi unavyowiwa naye; badala yake, lengo lake ni kujifunza kutumia roho, ikimwezesha kuutuliza moyo wake mbele za Mungu, kujifunza kutafuta mwongozo kutoka kwa maneno ya Mungu katika masuala yote, ili moyo wake uweze kukaribia mwanga mpya na safi kila siku, na ili mtu asiwe mwenye kukaa tu ama mzembe na aweze kuingia kwenye njia sahihi ya kuyaweka maneno ya Mungu katika vitendo. Watu wengi siku hizi wanalenga mbinu za utendaji, lakini hawafanyi hivyo ili kuufuatilia ukweli na kufanikisha ukuaji wa maisha. Hapa ndipo walipopotoka. Pia kuna wengine wanaoweza kupokea mwanga mpya, lakini mbinu zao za utendaji hazibadiliki. Wao hutumia fikira zao za kale wanapotazamia kupokea maneno ya

Mungu ya leo, kwa hivyo kile wanachopokea bado ni mafundisho yaliyoathiriwa na fikira za kidini; hawapokei mwanga wa leo hata kidogo. Kwa hiyo, matendo yao yametiwa doa; ni matendo yale yale ya kale katika kifurushi kipya. Bila kujali wanaweza kutenda vyema jinsi gani, wao ni wanafiki. Mungu huwaongoza watu katika kufanya mambo mapya kila siku, Akitaka kwamba kila siku wapate umaizi na ufahamu mpya, na kuwahitaji wasiwe waliopitwa na wakati na wenye kurudiarudia. Ikiwa umemwamini Mungu kwa miaka mingi, lakini mbinu zako za utendaji hazijabadilika hata kidogo, na ikiwa wewe bado ni mwenye raghba na mwenye shughuli nyingi kuhusu masuala ya nje, lakini huna moyo mtulivu wa kuleta mbele za Mungu ili uyafurahie maneno Yake, basi hutapata chochote. Inapofikia kuikubali kazi mpya ya Mungu, usipopanga kwa njia tofauti, usipotenda kwa njia mpya, na usifuatilie ufahamu wowote mpya, lakini badala yake ushikilie ya kale na kupokea tu mwanga finyu mpya, bila kubadili jinsi unavyotenda, basi watu kama wewe wako katika mkondo huu kwa jina tu; kwa kweli, wao ni Mafarisayo wa kidini walio nje ya mkondo wa Roho Mtakatifu.

Ili kuishi maisha ya kawaida ya kiroho, lazima mtu aweze kupokea mwanga mpya kila siku na afuatilie ufahamu wa kweli wa maneno ya Mungu. Ni lazima mtu aone ukweli vyema, apate njia ya utendaji katika masuala yote, agundue maswali mapya kupitia kusoma maneno ya Mungu kila siku, na atambue upungufu wake mwenyewe ili aweze kuwa na moyo unaotamani na kutafuta ambao unaigusa nafsi yake nzima, na ili aweze kutulia mbele za Mungu nyakati zote, akiogopa sana kubaki nyuma. Mtu aliye na moyo kama huu unaotamani na kutafuta, aliye tayari kupata kuingia bila kusita, yuko kwenye njia sahihi ya maisha ya kiroho. Wale wanaoguswa na Roho Mtakatifu, wanaotaka kufanya vizuri zaidi, walio tayari kufuatilia kukamilishwa na Mungu, wanaotamani ufahamu wa kina wa maneno ya Mungu, wasiofuatilia jambo la mwujiza lakini badala yake wanalipa gharama ya kweli, wanaoyajali mapenzi ya Mungu kwa kweli, ambao kwa kweli wanapata kuingia ili uzoefu wao uwe wa kweli na halisi zaidi, wasiofuatilia maneno na mafundisho matupu ama kufuatilia kuhisi jambo la mwujiza, wasiomwabudu mtu yeyote mashuhuri—hawa ndio wale ambao wameingia katika maisha ya kawaida ya kiroho. Kila kitu wanachofanya kinanuiwa kufanikisha ukuaji zaidi katika maisha na kuwafanya wawe wapya na wachangamfu katika roho, na daima wanaweza kupata kuingia kwa shauku. Bila wao kujua, wanakuja kuuelewa ukweli na kuingia katika uhalisi. Wale walio na maisha ya kawaida ya kiroho hupata ukombozi na uhuru wa roho kila siku, na wanaweza kutenda maneno ya Mungu kwa njia huru mpaka Aridhike. Kwa watu hawa, kuomba si jambo la kidesturi ama utaratibu; kila siku, wanaweza kuwa sambamba na mwanga mpya. Kwa mfano, watu hujifunza kuituliza mioyo yao mbele za Mungu, na mioyo yao inaweza kutulia mbele za Mungu kwa kweli, na hawawezi kusumbuliwa na yeyote. Hakuna mtu, tukio ama jambo linaloweza kuzuia maisha yao ya kawaida ya kiroho. Mafunzo kama hayo yananuiwa kuleta matokeo; hayanuiwi kuwafanya

watu wafuate kanuni. Utendaji huu hauhusu kufuata kanuni, lakini badala yake unahusu kukuza ukuaji katika maisha ya watu. Ikiwa unaona utendaji huu kuwa kanuni za kufuatwa tu, maisha yako hayatawahi kubadilika. Unaweza kuwa umeshiriki katika matendo sawa kama wengine, lakini wakati wao wanaweza hatimaye kuwa sambamba na kazi ya Roho Mtakatifu, unaondolewa kutoka katika mkondo wa Roho Mtakatifu. Je, hujidanganyi? Lengo la maneno haya ni kuwawezesha watu waitulize mioyo yao mbele za Mungu, waigeuze mioyo yao kumwelekea Mungu, ili kazi ya Mungu ndani yao iweze kutozuiwa na iweze kuzaa matunda. Ni baada ya hayo tu ndiyo watu wataweza kukubaliana na mapenzi ya Mungu.

Kujadili Maisha ya Kanisa na Maisha Halisi

Watu huhisi kuwa wao wanaweza tu kubadilika katika maisha ya kanisani. Iwapo hawako ndani ya maisha kanisa, wanahisi kwamba hawawezi kubadilika, kana kwamba mbadiliko hauwezi kutimika katika maisha halisi. Mwaweza kutambua suala hili ni lipi? Nimeongea juu ya kumleta Mungu katika maisha halisi, na hii ndiyo njia kwa wale wanaomwamini Mungu kuingia katika uhalisi wa maneno ya Mungu. Kwa kweli, maisha ya kanisa ni njia ndogo tu ya kuwakamilisha watu. Mazingira ya msingi ya kuwakamilisha wanadamu bado ni maisha halisi. Hiki ndicho kitendo halisi na mafunzo halisi Niliyozungumzia, yanayowaruhusu wanadamu kutimiza maisha ya ubinadamu wa kawaida na kuishi kwa kudhihirisha mfano wa mtu wa kweli katika maisha ya kila siku. Kipengele kimoja ni kwamba mtu lazima aelimike ili kuinua kiwango chake mwenyewe cha elimu, aweze kuelewa maneno ya Mungu, na kutimiza uwezo wa kuelewa. Kipengele kingine ni kwamba mtu lazima ajiandae na ujuzi wa msingi unaohitajika kuishi kama mwanadamu ili kutimiza ufahamu na busara ya ubinadamu wa kawaida, kwa sababu wanadamu wamepungukiwa sana katika sehemu hii takriban kwa ukamilifu. Aidha, mtu lazima pia aje kufurahia maneno ya Mungu kupitia kwa maisha ya kanisa, na polepole kupata ufahamu dhahiri wa ukweli.

Kwa nini husemwa kuwa katika kumwamini Mungu, mtu sharti amlete Mungu katika maisha halisi? Maisha ya kanisa hayawezi tu kumbadilisha mwanadamu, lakini muhimu zaidi, mwanadamu anapaswa kuingia katika uhalisi wa maisha halisi. Mlikuwa daima mkizungumzia hali yenu ya kiroho na masuala ya kiroho huku mkipuuza mafunzo katika mambo mengi katika maisha halisi, na pia kupuuza kuingia kwenu ndani yao. Mliandika kila siku, mkasikiliza kila siku, na mkasoma kila siku. Mliomba mlipokuwa mnapika: “Ee Mungu! Na uwe maisha yangu ndani yangu. Niipite siku hii namna gani? Tafadhali nibariki, nipe nuru. Lolote utakalonipa nuru kuhusu leo, tafadhali niruhusu kulielewa kwa wakati huu, ili maneno Yako yawe kama maisha yangu.” Ninyi pia mliomba mlipokuwa mnakula chajio: “Ee Mungu! Umetupatia sisi chakula hiki. Utubariki sisi. Amina! Tafadhali turuhusu kukutumainia Wewe kwa ajili ya maisha yetu.

Uwe nasi. Amina!” Baada ya kumaliza chajio chako na huku ukisafisha vyombo ukaanza kuparaganya tena: “Ee Mungu, mimi ni bakuli hii. Tumepotoshwa na Shetani na tuko tu kama mabakuli ambayo yametumika na ni lazima yaoshwe kwa maji. Wewe ndiwe maji, maneno Yako ndiyo maji yaliyo hai yanayotoa kwa maisha yangu.” Kufumba kufumbua, ilikuwa wakati wa kulala, na ulianza kuparaganya tena: “Ee Mungu! Umenibariki mimi na kuniongoza siku nzima. Ninakushukuru kwa dhati....” Hivi ndivyo ulitamatisa siku yako na kuingia kwenye usingizi. Watu wengi sana waliishi namna hii kila siku, na hata mpaka sasa, hawajazingatia kuingia halisi, ila wanasisitiza tu maneno matupu kwenye maombi yao. Haya ndiyo maisha ya awali ya mwanadamu—haya ndiyo maisha yao ya kale. Watu wengi sana wako hivi, wamekosa mafundisho yoyote halisi, na wana mabadiliko halisi machache sana. Wanatoa tu maneno matupu katika maombi yao, wakimwendea Mungu kwa maneno yao lakini wanakosa uketo katika ufahamu wao. Hebu tuchukue mfano rahisi zaidi—kusafisha nyumba yako. Unaona kuwa nyumba yako ni chafu, kwa hiyo unakaa hapo na kuomba: “Ee Mungu! Tazama upotovu ambao Shetani amegusisha kwangu. Mimi ni mchafu tu kama nyumba hii. Ee Mungu! Nakusifu na kukushukuru Wewe. Bila wokovu na nuru Yako, singetambua jambo hili.” Unakaa hapo tu na kuparaganya, ukiomba kwa muda mrefu, na kisha unajifanya kuwa hakuna kilichotendeka, ukitenda kama mwanamke mzee mwenye kusemasema ovyo. Unapitisha maisha yako ya kiroho hivi bila kuingia kokote kwa kweli katika uhalisi kabisa, na vitendo vingi sana vya kujipurukusha! Kuingia katika mafunzo halisi kunahusu maisha halisi ya watu na matatizo yao ya utendaji—hili tu ndilo linaweza kuwabadilisha. Pasipo maisha halisi, wanadamu hawawezi kubadilishwa. Kuna haja gani kutumia maneno matupu kwenye maombi yao? Bila kuelewa asili ya wanadamu, kila kitu ni kupoteza muda, na pasipo njia ya kutenda, kila kitu ni kupoteza juhudi! Maombi ya kawaida yanaweza kuwasaidia watu kudumisha hali zao za kawaida ndani ya watu, lakini hawawezi kubadilishwa kikamilifu nayo. Kujua kujidai, kiburi, majisifu, kujiona na tabia potovu ya binadamu—ujuzi wa mambo haya hauji kwa maombi, bali hutambulika kwa kufurahia maneno ya Mungu, na unajulikana kwa kupewa nuru na Roho Mtakatifu katika maisha halisi. Watu siku hizi wote huweza kuongea vizuri, na wamesikiza mahubiri ya juu sana, yaliyo juu sana kuliko mengine yoyote katika enzi, lakini ni kidogo mno yanayotekelezwa katika maisha yao halisi. Hivyo ni kusema, katika maisha halisi ya watu hakuna Mungu, na wanakosa maisha ya mtu mpya baada ya kubadilishwa. Hakuna kuishi kwa kudhihirisha ukweli katika maisha halisi, na hakuna kumleta Mungu katika maisha halisi. Maisha ya watu yanaendelezwa kana kwamba wao ni wana wa jehnamu. Je, huku si kupotoka dhahiri?

Ili kurudisha mfanano wa mtu wa kawaida, yaani, kutimiza ubinadamu wa kawaida, watu hawawezi tu kumpendeza Mungu kwa maneno yao. Wanajiumiza wenyewe kwa kufanya hivyo, na haileti faida yoyote kwa kuingia na kubadili kwao. Kwa hivyo, ili kufikia mbadiliko, watu

lazima watende kidogo kidogo, waingie taratibu, watafute na kuchunguza kidogo kidogo, waingie ndani kutoka kwa halisi, na kuishi maisha ya utendaji wa ukweli, maisha ya watakatifu. Tangu sasa kuendelea, inahusisha mambo halisi, vitu halisi, na mazingira halisi, kuwaruhusu watu kuwa na mafunzo ya utendaji. Haiwahitaji hao kutoa maneno matupu; badala yake, inahitaji mafunzo katika mazingira halisi. Watu huja kutambua kuwa wao ni wenye ubora duni wa tabia, na kisha wana kula na kunywa halisi kwa maneno ya Mungu halisi, kuingia halisi, na utandaji halisi, hivi ndivyo wanavyopokea uhalisi na hivi ndivyo kuingia kunaweza kufanyika hata haraka zaidi. Ili kuwabadili watu, lazima kuwe na utendaji, lazima wafanye mazoezi na mambo halisi, vitu halisi, na mazingira halisi. Kwa kutegemea tu maisha ya kanisa, inawezekana kutimiza mafunzo ya kweli? Je, mwanadamu angeingia katika uhalisi? La. Iwapo mwanadamu hawezi kuingia katika maisha halisi, basi yeye hawezi kubadili njia zake za zamani za kufanya mambo na kuishi maisha. Sio tu kwa sababu ya uvivu wa mwanadamu au utegemezi wake wa nguvu, bali ni kwa sababu mwanadamu hana uwezo wa kuishi, na zaidi, hana ufahamu wa kiwango cha mfanano wa mtu wa kawaida. Hapo kale, watu walikuwa daima wakiongea, wakinena, wakiwa na ushirika, hata wakawa “wanenaji hodari”; lakini hakuna yeyote kati yao alitafuta mabadiliko katika tabia ya maisha; walishikilia tu kutafuta nadharia za kina. Kwa hivyo, leo inapasa mbadili maisha haya ya kidini ya kumwamini Mungu. Lazima muingie ndani na kutenda kwa kulenga kitu kimoja, jambo moja, mtu mmoja. Lazima mfanye mambo na malengo—hapo tu ndio mtafikia matokeo. Ili kuwabadili watu, lazima kuanze na kiini chao. Kazi lazima ilenge kiini cha watu, maisha yao, uvivu, utegemezi, na utumwa wa watu, na kwa njia hii tu ndio wanaweza kubadilishwa.

Ijapokuwa maisha ya kanisa yanaweza kuleta matokeo katika sehemu nyingine, msingi bado ni kuwa maisha halisi yanaweza kuwabadilisha watu, na hali yao ya kale haiwezi kubadilika bila maisha halisi. Hebu tuchukue kazi ya Yesu katika Enzi ya Neema. Yesu alipoharamisha sheria za awali na kuanzisha amri za enzi mpya, Alinena kupitia mifano ya maisha halisi. Wakati Yesu Alipowaongoza wanafunzi wake kupita katika shamba la ngano siku ya Sabato, wanafunzi Wake walihisi njaa na wakatunda na kula masuke ya nafaka, Mafarisayo walipoona hivi walisema kuwa hawakuitii Sabato. Pia walisema kuwa watu hawakuruhusiwa kuwaokoa ndama walioanguka shimoni katika siku ya Sabato, wakisema kuwa hakuna kazi ingepaswa kufanywa wakati wa Sabato. Yesu alitumia matukio haya ili kutangaza rasmi amri za enzi mpya hatua kwa hatua. Wakati huo, Alitumia mambo mengi ya kiutendaji ili watu waelewe na kubadilika. Hii ndiyo kanuni ambayo kwayo Roho Mtakatifu hutekeleza kazi Yake, na ni njia hii pekee inayoweza kubadili watu. Wanapokosa mambo ya kiutendaji, watu wanaweza tu kupata ufahamu katika nadharia na wanaweza kuelewa tu mambo kiakili—hii si njia ya kufaa kubadili watu. Tukiongea juu ya kupata busara na ufahamu kupitia mafundisho, hili

lingetimizwaje? Je, mwanadamu angeweza kupata busara na ufahamu kwa kusikiza, kusoma na kukuza ujuzi wake tu? Je, hili linasababishaje kupata busara na ufahamu? Mtu lazima afanye bidii kuelewa na kuwa na uzoefu kupitia maisha halisi. Kwa hivyo, mafunzo hayawezi kukosa na mtu hawezi kuacha maisha halisi. Mtu lazima azingatie hali tofauti na aingie kwa hali mbalimbali: kiwango cha elimu, ufafanuzi, uwezo wa kuona mambo, utambuzi, uwezo wa kuelewa maneno ya Mungu, maarifa ya kawaida na kanuni za ubinadamu, na vitu vingine vinavyohusiana na ubinadamu ambavyo mtu lazima awe navyo. Baada ya ufahamu kufikiwa, mtu lazima alenge kuingia, na hapo tu ndio mabadiliko yanaweza kufikiwa. Iwapo mwanadamu amefikia ufahamu lakini anakaidi utendaji, mabadiliko yanawezaje kutokea? Sasa, mwanadamu amefahamu mengi, lakini haishi kwa kudhihirisha uhalisi, hivyo basi anaweza kuwa tu na ufahamu halisi kidogo wa maneno ya Mungu. Umepata nuru kwa kiasi kidogo, umepokea mwangaza kidogo kutoka kwa Roho Mtakatifu, lakini huna kuingia katika maisha halisi, au hata huenda hujali juu ya kuingia, hivyo basi utakuwa na mabadiliko kidogo tu. Baada ya muda mrefu hivyo, watu wameelewa mengi na wanaweza kusema mengi juu ya ujuzi wao wa nadharia, lakini tabia yao ya nje husalia ile ile, na ubora wa tabia yao wa asili hudumu bila upandaji hadhi hata kidogo. Iwapo mambo yako hivi, mtaingia lini humo hatimaye?

Maisha ya kanisa ni aina ya maisha tu ambapo watu hukutana kufurahia maneno ya Mungu, na huchukua tu kipande kidogo cha maisha ya mtu. Iwapo maisha halisi ya watu yangukuwa kama maisha yao ya kanisani—ikiwemo maisha ya kawaida ya kiroho, kufurahia maneno ya Mungu kwa kawaida, kuomba na kuwa karibu na Mungu kwa kawaida, kuishi maisha halisi ambapo kila kitu kinatekelezwa kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu, kuishi maisha halisi ambapo kila kitu kinatekelezwa kwa mujibu wa ukweli, kuishi maisha halisi ya kutekeleza maombi na kuwa kimya mbele ya Mungu, ya kufanya mazoezi ya kuimba nyimbo za kidini na kucheza, maisha kama haya tu yangemleta mtu katika maisha ya maneno ya Mungu. Watu wengi sana hulenga tu masaa kadhaa ya maisha yao ya kanisa bila “kutunza” maisha yao nje ya masaa hayo, kana kwamba hayahusiki nao. Pia kuna watu wengi ambao huingia tu katika maisha ya watakatifu wanapokula na kunywa maneno ya Mungu, wakiimba nyimbo za kidini au wakiomba, kisha hurejelea nafsi zao za kale nje ya nyakati hizo. Maisha kama hayo hayawezi kubadili watu, na hayatawaruhusu kumjua Mungu. Katika kumwamini Mungu, iwapo mwanadamu anataka mabadiliko kwa tabia yake mwenyewe, basi lazima asijitenge na maisha halisi. Katika maisha halisi, lazima ujijue mwenyewe, ujitelekeze mwenyewe, utende ukweli, na vilevile kujifunza kanuni, maarifa ya kawaida na masharti ya kujiendesha katika mambo yote kabla ya wewe kuweza kutimiza mabadiliko ya polepole. Iwapo utalenga tu ujuzi katika nadharia na kuishi tu katika sherehe za dini bila ya kuingia ndani ya uhalisi, bila kuingia kwenye maisha halisi, basi hutaweza kamwe kuingia katika uhalisi, hutaweza kujijua mwenyewe, kuujua ukweli, au kumjua

Mungu, na utakuwa kipofu na mjinga milele. Kazi ya Mungu ya kuwaokoa watu sio kuwaruhusu waishi maisha ya kawaida ya binadamu baada ya kipindi cha muda mfupi, na wala sio ili kubadili mawazo na mafundisho yao yasiyo sahihi. Badala yake, kusudi Lake ni kubadili tabia za zamani za watu, kubadilisha kikamilifu njia yao ya zamani ya maisha, na kubadilisha njia zao zote za mawazo na mtazamo wa akili zilizopitwa na wakati. Kulenga tu maisha ya kanisa pekee hakuwezi kubadili mazoea ya kale ya watu au kubadili njia za kale walizoishi kwa muda mrefu. Lolote litokealo, watu hawapaswi kujitenga na maisha halisi. Mungu anauliza kwamba watu waishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida katika maisha halisi, sio tu katika maisha ya kanisani; kwamba waishi kwa kudhihirisha ukweli katika maisha halisi, sio tu katika maisha ya kanisani; kwamba watimize majukumu yao katika maisha halisi, sio tu katika maisha ya kanisani. Ili kuingia katika uhalisi, mtu lazima apindue vitu vyote kuelekea maisha halisi. Iwapo waumini katika Mungu, watu hawawezi kuja kujijua kupitia kuingia katika maisha halisi, na ikiwa hawawezi kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida katika maisha halisi, watahindwa. Wale wanaomkaidi Mungu wote ni watu ambao hawawezi kuingia katika maisha halisi. Wote ni watu wanaozungumza kuhusu ubinadamu lakini wanaishi kwa kudhihirisha asili ya pepo mbaya. Wote ni watu wanaozungumza kuhusu ukweli lakini wanaishi kwa kudhihirisha kanuni badala yake. Wale wasioweza kuishi kwa kudhihirisha ukweli katika maisha halisi ni wale wanaoamini katika Mungu lakini wanachukiwa na kukataliwa na Yeye. Lazima ufanye mazoezi ya kuingia kwako katika maisha halisi, ujue upungufu wako mwenyewe, ukaidi na upumbavu, na ujue ubinadamu wako usio wa kawaida na udhaifu. Kwa njia hiyo, ufahamu wako wote utaambatanishwa ndani ya hali yako halisi na ugumu. Ni aina hii ya ufahamu pekee ndiyo ya kweli na inaweza kukufanya ushike kwa hakika hali yako mwenyewe na ufanikishe mabadiliko ya tabia yako.

Sasa kwa vile kukamilishwa kwa mwanadamu kumeanza rasmi, mtu lazima aingie katika maisha halisi. Kwa hivyo, ili kutimiza mabadiliko, lazima mtu aanzie kwa kuingia katika maisha halisi, na kubadilika kidogo kidogo. Ukihepa maisha ya kawaida ya binadamu na kuongea tu kuhusu mambo ya kiroho, basi mambo hugeuka makavu na bapa, hugeuka yasiyo ya uhalisi, na mtu angebadilika vipi? Sasa unaambiwa uingie katika maisha halisi kufanya mazoezi, ili uweze kuweka msingi wa kuingia katika uzoefu wa kweli. Hii ni mojawapo ya mambo ambayo mtu anapaswa kufanya. Kazi ya Roho Mtakatifu hasa ni kuongoza, ilhali iliyosalia hutegemea utendaji wa watu na kuingia. Kila mmoja anaweza kufikia kuingia katika maisha halisi kwa njia mbalimbali, kiasi kwamba wanaweza kumleta Mungu katika maisha halisi, na kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida halisi. Haya tu ndiyo maisha yenye maana!

Kuhusu Kila Mmoja Kutekeleza Wajibu Wake

Katika mkondo wa sasa, kila mtu anayempenda Mungu kwa kweli ana fursa ya kukamilishwa na Yeye. Bila kujali kama yeye ni kijana au mzee, mradi tu anatazamia kwa hamu kumtii Mungu na kumheshimu Yeye, wataweza kukamilishwa na Yeye. Mungu huwakamilisha watu kulingana na kazi zao tofauti. Mradi tu umefanya yote kwa nguvu yako na kuitii kazi ya Mungu utakuwa na uwezo wa kukamilishwa na Yeye. Kwa sasa hakuna hata mmoja wenu aliye mkamilifu. Wakati mwingine mnaweza kutekeleza aina moja ya kazi na wakati mwingine mnaweza kutekeleza mbili; mradi tu mnatoa nguvu zenu zote kujitumia kwa ajili ya Mungu, hatimaye mtafanywa wakamilifu na Mungu.

Vijana wana falsafa chache za maisha, na hawana hekima na ufahamu. Mungu amekuja hapa kukamilisha hekima na ufahamu wa mwanadamu, na neno la Mungu huyafidia mambo haya ambayo hawana. Hata hivyo, tabia za vijana si thabiti na hii inahitaji mbadiliko na Mungu. Vijana wana mawazo machache ya kidini na falsafa chache za maisha Wanafikiri kwa maneno rahisi, na fikira zao sio ngumu kufahamika. Hiki ni kipengele ambacho ubinadamu wao bado haujachukua umbo na ni kipengele cha kupendeza, lakini vijana hawajui na hawana hekima, na hii ni sehemu ambayo inahitaji kukamilishwa na Mungu. Kupitia kukamilishwa na Mungu, mnaweza kukuza utambuzi na kuweza kuelewa mambo mengi ya kiroho, na hatua kwa hatua mgeuke kuwa watu wanaostahili kutumiwa na Mungu. Ndugu na dada wakubwa pia wanaweza kutekeleza kazi fulani na hawajaachwa na Mungu. Na ndugu na dada wakubwa, wao pia wana mambo yanayofaa na baadhi ya mambo yasiyofaa. Ndugu na dada wakubwa wana falsafa zaidi za maisha, wana mawazo zaidi ya kidini, vitendo vyao vimekwama katika mfumo usiopindika, hufuata sheria kama roboti, wao huvitumia bila kufikiri, na hawawezi kubadilika. Hiki sicho kipengele kinachofaa. Hata hivyo, ndugu na dada wakubwa ni watulivu na wenye kijidhibiti nafsi kuelekea chochote kinachojitokeza; tabia zao ni imara, na hawana hisia kali zisizoweza kutabiriwa. Wanaweza kuwa wapole katika kukubali mambo, lakini hii siyo kasoro kubwa. Mradi mnaweza kutii; mradi mnaweza kuyakubali maneno ya sasa ya Mungu, ikiwa hamchunguzi maneno ya Mungu, ikiwa hamsiti kutii na kufuata, ikiwa hakika hutoi hukumu au kuwa na mawazo mengine mabaya, na ikiwa mnakubali maneno Yake na kuyaweka katika matendo—ikiwa mnakidhi hali hizi—mtaweza kukamilishwa.

Bila kujali kama ninyi ni ndugu au dada wadogo au wakubwa, mnajua kazi mnayopaswa kutekeleza. Wale walio katika ujana wao sio wenye kiburi; wale walio wakubwa zaidi sio wasioonyesha hisia na hawarudi nyuma. Nao wanaweza kutumia nguvu za kila mmoja kufidia upungufu wao, na wanaweza kuhudumiana bila ubaguzi wowote. Daraja la urafiki linajengwa kati ya ndugu na dada wadogo na wakubwa. Kwa sababu ya upendo wa Mungu mnaweza kuelewana vizuri zaidi. Ndugu wadogo hawawadharau ndugu wakubwa, na ndugu wakubwa sio wa kujidai. Je! Huu si ushirikiano patanifu? Ikiwa ninyi nyote mna uamuzi huu, basi mapenzi ya

Mungu hakika yatatimizwa katika kizazi chenu.

Katika siku zijazo, ikiwa wewe unabarikiwa au kulaaniwa kutaamuliwa kulingana na matendo unayotekeleza leo. Ikiwa unafaa kukamilishwa na Mungu itakuwa ni sasa hivi katika enzi hii; hakutakuwa na fursa nyingine katika siku zijazo. Mungu kwa kweli Anataka kukukamilisha sasa, na hii sio njia ya kuzungumza. Katika siku zijazo, bila kujali majaribio gani yanayokufikia, matukio gani yanayofanyika, au maafa gani yanayokupata, Mungu anataka kukukamilisha—huu ni ukweli wa hakika na usio na shaka. Je, jambo hili inaweza kuonekana kutoka wapi? Kutokana na ukweli kwamba neno la Mungu katika enzi zote na vizazi halijawahi kufikia kiwango kikubwa kama lilivyo leo—limeingia katika ulimwengu wa juu, na kazi ya Roho Mtakatifu miongoni mwa wanadamu leo ni ya kipekee. Ni wachache sana kutoka vizazi vilivyopita wameonja hili. Hata katika enzi ya Yesu hapakuwa na ufunuo wa leo; viwango vikubwa vimefikiwa katika maneno yaliyosemwa kwenu, mambo mnayoyaelewa, na mambo mnayoyapitia. Hamuondoki katikati ya majaribu na kuadibiwa, na hii ni inatosha kuthibitisha kwamba kazi ya Mungu imefikia uzuri ambao haujawahi kutokea. Hiki si kitu ambacho mwanadamu anaweza kufanya na sio kitu ambacho mwanadamu anadumisha, lakini badala yake ni kazi ya Mungu Mwenyewe. Kwa hivyo, kutokana na ukweli mwingi wa kazi ya Mungu inaweza kuonekana kwamba Mungu anataka kumkamilisha mwanadamu, na Yeye hakika Anaweza kukufanya uwe mkamilifu. Ikiwa mnaweza kuona jambo hili, ikiwa unaweza kupata ugunduzi huu mpya, basi hutangoja kuja kwa pili kwa Yesu lakini badala yake, utamruhusu Mungu akufanye mkamilifu katika enzi ya sasa. Hivyo, kila mmoja wenu anapaswa kufanya kila linalowezekana na kujitahidi sana ili aweze kukamilishwa na Mungu.

Siku hizi hupaswi kuzingatia mambo hasi. Lazima kwanza uweke kando na kutojali kila kitu ambacho kinaweza kukufanya usihisi hasi. Unaposhughulikia mambo lazima udumishe moyo wa kutafuta na kupapasa papasa, na lazima udumishe moyo wa utii kwa Mungu. Wakati wowote mnapogundua udhaifu wowote ndani yenu, lakini hamko chini ya udhibiti wake na mnatenda kazi ambayo mnapaswa kutenda, hii ni hatua ya hakika kwenda mbele. Kwa mfano: Ndugu wana mawazo ya kidini, lakini unaweza kuomba, na unaweza kutii, kula na kunywa neno la Mungu, na kuimba nyimbo.... Kwa neno moja, chochote unachoweza kufanya, kazi yoyote unayoweza kutenda, jitolee kikamilifu kwa nguvu zote unazoweza kuzitumia. Usisubiri kwa kukaa tu. Kuweza kutimiza wajibu wako kwa ridhaa ya Mungu ni hatua ya kwanza. Kisha unapoweza kuuelewa ukweli na kuingia katika ukweli wa neno la Mungu, utakuwa umekamilishwa na Mungu.

Kuhusu Mungu Kumtumia Mwanadamu

Hakuna mtu anayeweza kuishi kwa kujitegemea isipokuwa wale ambao wanapewa uelekeo

na mwongozo maalumu na Roho Mtakatifu, kwani wanahitaji huduma na uchungaji wa wale wanaotumiwa na Mungu. Hivyo, katika kila enzi Mungu huwainua watu tofauti ambao hujishughulisha na kuchunga makanisa kwa ajili ya kazi Yake. Ambalo ni kusema, kazi ya Mungu lazima ifanywe kupitia wale ambao Huwaonyesha fadhili na kuwakubali; Roho Mtakatifu lazima atumie sehemu ndani yao inayostahili kutumiwa ili kufanya kazi, na wao hufanywa wa kufaa kutumiwa na Mungu kupitia kukamilishwa na Roho Mtakatifu. Kwa sababu uwezo wa mwanadamu wa kuelewa unapungukiwa sana, lazima afanyiwe uchungaji na wale wanaotumiwa na Mungu; ilikuwa vivyo hivyo na Mungu kumtumia Musa, ambaye kwake Alipata mengi yaliyostahili kwa matumizi wakati huo, na ambayo Aliyatumia kufanya kazi ya Mungu wakati wa hatua hiyo. Katika hatua hii, Mungu anamtumia mwanadamu huku Akitumia pia kwa manufaa Yake sehemu yake inayoweza kutumiwa na Roho Mtakatifu ili kufanya kazi, na Roho Mtakatifu humwongoza na wakati ule ule hukamilisha sehemu iliyobaki, isiyoweza kutumika.

Kazi inayotekelezwa na yule anayetumiwa na Mungu ni kwa ajili ya kushirikiana na kazi ya Kristo au Roho Mtakatifu. Mtu huyu anainuliwa na Mungu miongoni mwa wanadamu, yuko pale kuongoza wateule wote wa Mungu, na pia yeye anainuliwa na Mungu ili kufanya kazi ya ushirikiano wa mwanadamu. Na mtu kama huyu, ambaye anaweza kufanya kazi ya ushirikiano wa mwanadamu, matakwa mengi zaidi ya Mungu kwa mwanadamu na kazi ambayo Roho Mtakatifu lazima Afanye miongoni mwa wanadamu inaweza kutimizwa kupitia kwake. Njia nyingine ya kulisema ni hivi: Lengo la Mungu katika kumtumia mtu huyu ni ili wote wanaomfuata Mungu waweze kuelewa bora mapenzi ya Mungu, na waweze kufikia matakwa zaidi ya Mungu. Kwa vile watu hawawezi kuyaelewa maneno ya Mungu na mapenzi ya Mungu moja kwa moja, Mungu amemuinua mtu fulani ambaye anatumia kutekeleza kazi kama hiyo. Mtu huyu anayetumiwa na Mungu anaweza kuelezwa kama chombo ambacho Mungu hutumia kuwaongoza watu, kama “mfasiri” anayewasiliana kati ya Mungu na watu. Hivyo, mtu kama huyo hayuko kama yeyote kati ya wale wanaofanya kazi katika nyumba ya Mungu au ambao ni mitume Wake. Kama wao, anaweza kusemekana kuwa mtu anayemhudumia Mungu, lakini katika kiini cha kazi yake na usuli wa kutumiwa kwake na Mungu anatofautiana sana na wafanyakazi wengine na mitume. Kuhusu kiini cha kazi yake na usuli wa kutumiwa kwake, mwanadamu anayetumiwa na Mungu huinuliwa na Yeye, hutayarishwa na Mungu kwa kazi ya Mungu, na yeye hushirikiana katika kazi ya Mungu Mwenyewe. Hakuna mtu anayeweza kufanya kazi yake badala yake—huu ni ushirikiano wa mwanadamu ambao ni wa lazima pamoja na kazi takatifu. Kazi inayotekelezwa na wafanyakazi wengine au mitume, wakati ule ule, ni uchukuzi na utekelezaji tu wa hali nyingi za matayarisho ya makanisa wakati wa kila kipindi, ama sivyo kazi ya utoaji wa kawaida wa uzima ili kudumisha uzima wa kanisa. Wafanyakazi

hawa na mitume hawateuliwi na Mungu, seuze kuweza kuitwa wale wanaotumiwa na Roho Mtakatifu. Wao huchaguliwa kutoka miongoni mwa makanisa na, baada ya kufunzwa na kukuzwa kwa kipindi cha wakati, wale wanaofaa hubaki, huku wale wasiofaa hurudishwa walikotoka. Kwa vile watu hawa huchaguliwa kutoka miongoni mwa makanisa, wengine huonyesha tabia yao halisi baada ya kuwa viongozi, na wengine hata hufanya mambo mengi mabaya na huishia kufutwa. Mtu anayetumiwa na Mungu, kwa upande mwingine, ni mtu ambaye ametayarishwa na Mungu, na aliye na ubora fulani wa tabia, na ana ubinadamu. Ametayarishwa na kukamilishwa mapema na Roho Mtakatifu, na anaongozwa kabisa na Roho Mtakatifu, na, inapofikia kazi yake hasa, yeye huongozwa na kuamriwa na Roho Mtakatifu—kutokana na hilo hakuna mkengeuko katika njia ya kuwaongoza wateule wa Mungu, kwani Mungu kwa hakika huwajibikia kazi Yake mwenyewe, na Mungu hufanya kazi Yake nyakati zote.

Punde Unapoelewa Ukweli, Unapaswa Kuuweka Katika Vitendo

Kazi na neno la Mungu vinanuiwa kusababisha badiliko katika tabia yenu; lengo Lake si tu kuwafanya muelewe ama mjue kazi na neno Lake. Hilo halitoshi. Wewe ni mtu aliye na uwezo wa kufahamu, kwa hivyo hupaswi kuona ugumu kuelewa neno la Mungu, kwa sababu maneno mengi ya Mungu yameandikwa katika lugha ya mwanadamu, na Anazungumza kwa uwazi sana. Kwa mfano, unaweza kabisa kujifunza ni nini ambacho Mungu angetaka uelewe na utende; hili ni jambo ambalo mtu wa kawaida aliye na uwezo wa kufahamu anapaswa kuweza kufanya. Hasa, maneno ambayo Mungu anasema katika hatua ya sasa ni ya wazi na dhahiri zaidi, na Mungu anaonyesha mambo mengi ambayo watu hawajayazingatia, na vilvile kila aina ya hali za binadamu. Maneno Yake yanajumuisha yote na ni dhahiri kama mwanga wa mwezi kamili. Kwa hivyo sasa, watu wanaelewa masuala mengi, lakini bado kuna kitu kinachokosa—watu kuweka neno Lake katika vitendo. Ni lazima watu wapitie vipengele vyote vya ukweli kwa utondoti, na wauchunguze na kuutafuta kwa kina zaidi, badala ya kusubiri tu kufyonza chochote wanachopewa; vinginevyo wanakuwa kupe tu. Wanajua neno la Mungu, lakini hawaliweki katika vitendo. Mtu wa aina hii hapendi ukweli na mwishowe ataondolewa. Ili kuwa kama Petro wa miaka ya tisini, hili linamaanisha kwamba kila mmoja wenu anapaswa kutenda neno la Mungu, aingie kwa kweli katika yale unayoyapitia na apate nuru hata zaidi na kubwa zaidi katika ushirikiano wake na Mungu, ambao utakuwa wa msaada unaozidi daima kwa maisha yenu mwenyewe. Ikiwa mmesoma maneno mengi ya Mungu lakini mnaelewa tu maana ya maandiko na hamna maarifa ya moja kwa moja ya neno la Mungu kupitia uzoefu wenu halisi, basi hutajua neno la Mungu. Kwa kadiri inavyokuhusu, neno la Mungu si uzima, bali tu nyaraka zisizovutia.

Na ikiwa unaishi tu kwa kufuata nyaraka zisizovutia, basi huwezi kuelewa asili ya neno la Mungu wala hataelewa mapenzi Yake. Ni wakati tu ambapo unapitia neno Lake katika matukio yako halisi ndipo maana ya kiroho ya neno la Mungu itafichuka kwako, na ni kupitia uzoefu tu ndiyo unaweza kuelewa maana ya kiroho ya ukweli mwingi na ufungue siri za neno la Mungu. Usipouweka katika vitendo, basi bila kujali jinsi neno Lake lilivyo dhahiri, yote uliyoelewa ni nyaraka na mafundisho matupu tu, ambayo yamekuwa kanuni za kidini kwako. Je, Mafarisayo hawakufanya hivi? Mkitenda na kupitia neno la Mungu, linakuwa la utendaji kwenu; usipotafuta kulitenda, basi neno la Mungu kwako ni hekaya ya mbinguni ya tatu tu. Kwa kweli, mchakato wa kumwamini Mungu ni mchakato wa ninyi kupitia neno Lake na vilevile kupatwa na Yeye, ama kuzungumza dhahiri zaidi, kumwamini Mungu ni kuwa na maarifa na ufahamu wa neno Lake na kupitia na kuishi kwa kudhihirisha neno Lake; huu ndio uhalisi wa ninyi kumwamini Mungu. Ikiwa mnamwamini Mungu na mnatumai kupata uzima wa milele bila kutafuta kutenda neno la Mungu kama kitu kilicho ndani yenu, basi ninyi ni wapumbavu. Hii itakuwa sawa na kwenda katika karamu na kuangalia tu chakula na kujua na kuweza kuvikariri vitu vitamu bila kuvionja kwa kweli. Je, mtu kama huyu si mpumbavu?

Ukweli ambao mwanadamu anahitaji kuwa nao unapatikana katika neno la Mungu, na ni ukweli wenye manufaa na usaidizi zaidi kwa wanadamu. Ni dawa na ruzuku ambayo miili yenu inahitaji, kitu kinachomsaidia mwanadamu kurejesha tena ubinadamu wake wa kawaida. Ni ukweli ambao mwanadamu anapaswa kujitayarisha nao. Kadiri mnavyotenda neno la Mungu, ndivyo maisha yenu yatakavyositawi haraka zaidi, na ndivyo ukweli utakavyokuwa dhahiri zaidi. Mnapozidi kukua katika kimo, mtaona vitu vya dunia ya kiroho kwa dhahiri zaidi, na ndivyo mtakavyokuwa na nguvu zaidi kumshinda Shetani. Ukweli mwingi ambao hamwelewi utafanywa kuwa dhahiri mtakapotenda neno la Mungu. Watu wengi wanaridhishwa kuelewa tu maandiko ya neno la Mungu na hawalengi kujitayarisha kwa mafundisho badala ya kuzidisha uzoefu wao kwa vitendo, lakini, je, hiyo si njia ya Mafarisayo? Kwa hivyo msemu “Neno la Mungu ni uzima” unawezaje kuwa wa kweli kwao? Maisha ya mtu hayawezi kukua kwa kusoma neno la Mungu tu, bali ni wakati tu neno la Mungu linawekwa katika vitendo. Ikiwa unaamini kwamba kuelewa neno la Mungu ndicho kitu pekee kinachohitajika kuwa na uzima na kimo, basi ufahamu wako umepotoka. Kuelewa neno la Mungu kwa kweli hutokea unapoweka ukweli katika vitendo, na ni lazima uelewe kwamba “ni kwa kutenda ukweli tu ndipo unaweza kueleweka.” Leo, baada ya kusoma neno la Mungu, unaweza tu kusema kwamba unajua neno la Mungu, lakini huwezi kusema kwamba unalielewa. Wengine husema kwamba njia ya pekee ya kutenda ukweli ni kuuelewa kwanza, lakini hii ni sahihi kwa kiwango fulani tu, na hakika si sahihi kikamilifu. Kabla uwe na maarifa ya ukweli fulani, hujapitia ukweli huo. Kuhisi kwamba unaelewa kitu unachosikia katika mahubiri si kuelewa kwa kweli—huku ni kuwa na maneno

halisi ya ukweli tu, na si sawa na kuelewa maana ya kweli ndani yake. Kuwa tu na maarifa ya juujuu ya ukweli hakumaanishi kwamba kweli unauelewa ama una maarifa yoyote kuuhusu; maana ya kweli ya ukweli hutokana na kuupitia. Kwa hiyo, ni wakati tu unapopitia ukweli ndiyo unaweza kuuelewa, na ni hapo tu ndiyo unaweza kufahamu sehemu zake zilizofichika. Kukuza uzoefu wako ndiyo njia ya pekee ya kuelewa vidokezo, na kuelewa asili ya ukweli. Kwa hiyo, unaweza kuenda popote ukiwa na ukweli, lakini iwapo hakuna ukweli ndani yako, basi usifikirie kujaribu kuwashawishi hata wanafamilia wako sembuse watu wa kidini. Bila ukweli wewe ni kama vipande vidogo sana vya theluji vinavyopepea. lakini ukiwa na ukweli unaweza kuwa na furaha na uhuru, na hakuna anayeweza kukushambulia. Bila kujali jinsi nadharia fulani ilivyo thabiti, haiwezi kuushinda ukweli. Kukiwa na ukweli, dunia yenyewe haiwezi kuyumba na milima na bahari kusogezwa, wakati ukosefu wa ukweli unaweza kusababisha nyuta zenye nguvu za mji kuangushwa na mabuu. Huu ni ukweli dhahiri.

Katika hatua ya sasa, ni muhimu sana kujua ukweli kwanza, na kisha kuuweka katika vitendo na kujitayarisha zaidi na maana ya kweli ya ukweli. Mnapaswa kutafuta kupata hili. Badala ya kutafuta tu kuwafanya wengine wafuate maneno yako, unapaswa kuwasababisha wafuate vitendo vyako. Ni kwa njia hii pekee ndiyo unaweza kupata kitu cha maana. Bila kujali kitakachokukumba, bila kujali utakutana na nani, alimradi una ukweli, utaweza kusimama imara. Neno la Mungu ndicho kitu kimleteacho mwanadamu uzima, si kifo. Ikiwa baada ya kusoma neno la Mungu huchangamki, bali bado wewe ni mfu, basi una kasoro. Ikiwa baada ya muda fulani umesoma maneno mengi ya Mungu, na umesikiza mahubiri mengi ya vitendo, lakini bado uko katika hali ya kifo, basi hili ni thibitisho kwamba wewe si mtu anayethamini ukweli, wala wewe si mtu anayefuatilia ukweli. Ikiwa kweli mnetafuta kumpata Mungu, hamngelenga kujitayarisha na mafundisho na kutumia mafundisho ya juu sana kuwafunza wengine, lakini badala yake mngelenga kupitia neno la Mungu na kuweka ukweli katika vitendo. Je, hampaswi kutafuta kuingia katika hili sasa?

Mungu ana muda mdogo wa kufanya kazi Yake ndani ya mwanadamu, kwa hivyo kunaweza kuwa na matokeo yapi ikiwa hushirikiani na Yeye? Mbona Mungu daima anawataka mtende neno Lake punde mnapolielewa? Ni kwa sababu Mungu amewafichulia maneno Yake, na hatua yenu ifuatayo ni kuyatenda kwa kweli. Mnapotenda maneno haya, Mungu atatekeleza kazi ya nuru na mwongozo. Hivi ndivyo inavyopaswa kufanywa. Neno la Mungu linamwezesha mwanadamu asitawi maishani na asiwe na dalili zozote zinavyoweza kumsababisha mwanadamu apotoke ama asionyeshe hisia. Unasema umesoma neno la Mungu na umelitenda, lakini bado hujapokea kazi yoyote kutoka kwa Roho Mtakatifu. Maneno yako yanaweza tu kumpumbaza mtoto. Huenda watu wengine wasijue ikiwa dhamira zako ni njema, lakini, je, unafikiri kwamba inawezekana Mungu asijue? Ni kwa nini wengine wanatenda neno la Mungu na kupokea nuru ya

Roho Mtakatifu, lakini unatenda neno Lake na hupokei nuru ya Roho Mtakatifu? Je, Mungu ana mhemuko? Ikiwa dhamira zako kweli ni njema na wewe ni wa kushirikiana, basi Roho wa Mungu atakuwa nawe. Watu wengine daima hutaka kuonyesha utawala wao wenyewe, lakini kwa nini Mungu hawaruhusu wainuke na kuliongoza kanisa? Watu wengine wanatimiza kazi zao na kutenda wajibu wao tu, lakini kufumba na kufumbua, wamepata idhini ya Mungu. Hilo linawezekanaje? Mungu huchunguza moyo wa ndani sana wa mwanadamu, na watu wanaofuatilia ukweli lazima wafanye hivyo kwa dhamira njema. Watu wasio na dhamira njema hawawezi kusimama imara. Kimsingi kabisa, lengo lenu ni kuacha neno la Mungu lifanye kazi ndani yenu. Yaani, ni kuwa na ufahamu wa kweli wa neno la Mungu mnapolitenda. Pengine uwezo wenu wa kufahamu neno la Mungu ni duni, lakini unapotenda neno la Mungu, Anaweza kurekebisha dosari hii, kwa hivyo hampaswi tu kujua ukweli mwingi, lakini pia lazima muutende. Hili ni lengo kubwa zaidi ambalo haliwezi kupuuzwa. Yesu alivumilia fedheha nyingi na mateso mengi katika maisha Yake ya miaka thelathini na tatu na nusu. Aliteseka sana kwa sababu tu Alitenda ukweli, alifanya mapenzi ya Mungu katika vitu vyote, na alijali tu mapenzi ya Mungu. Haya yalikuwa mateso ambayo Hangepitia iwapo Angejua ukweli bila kuutenda. Ikiwa Yesu angefuata mafundisho ya Wayahudi na awafuate Mafarisayo, basi Hangeteseka. Unaweza kujifunza kutoka kwa matendo ya Yesu kwamba ufanisi wa kazi ya Mungu kwa mwanadamu hutokana na ushirikiano wa mwanadamu, na hili ni jambo ambalo lazima mtambue. Je, Yesu angeteseka jinsi Alivyoteseka msalabani ikiwa Hangetenda ukweli? Je, Angesali sala ya huzuni sana kama Hangetenda kulingana na mapenzi ya Mungu? Kwa hiyo, mnapaswa kuteseka kwa ajili ya kutenda ukweli; mtu anapaswa kupitia mateso ya aina hii.

Mtu Anayepata Wokovu ni Yule Ambaye Yuko Tayari Kutenda Ukweli

Umuhimu wa kuwa na maisha sahihi ya kanisa unatajwa mara kwa mara katika mahubiri. Kwa hivyo ni kwa nini maisha ya kanisa hayajaboreka bado, na bado ni yale yale ya zamani? Mbona hakuna njia mpya na tofauti kabisa ya maisha? Je, inaweza kuwa kawaida kwa mtu wa miaka ya tisini kuishi kama mfalme wa enzi iliyopita? Ingawa vitu ambavyo watu wanakula na kunywa sasa ni vyakula vitamu vilivyoondjwa mara chache katika enzi zilizopita, hakuja kuwa na mabadiliko makubwa katika maisha ya kanisa. Imekuwa kama kutia divai ya kale ndani ya viriba vipya. Je, kuna haja gani basi ya Mungu kusema mengi sana? Mekanisa katika maeneo mengi hayajabadilika hata kidogo. Mimi nimeona hili kwa macho Yangu Mwenyewe na ni wazi katika moyo Wangu; hata ingawa sijapitia maisha ya kanisa Mimi Mwenyewe, Nazijua hali za mikusanyiko ya kanisa vizuri sana. Hawajafanya maendeleo mengi. Inarejelea msembo huo—ni kama kutia divai ya kale ndani ya viriba vipya. Hakuna kilichobadilika! Wakati mtu

anapowachunga, wao huwaka kama moto, lakini wakati ambapo hakuna mtu wa kuwafadhili, wao ni kama pande kubwa la barafu. Si wengi wanaoweza kuzungumza juu ya mambo ya vitendo, na ni mara chache ambapo mtu yeyote anaweza kushika usukani. Ingawa mahubiri ni ya juu, imekuwa nadra kwa mtu yeyote kupata kuingia. Watu wachache huthamini neno la Mungu. Wao hujawa na machozi wanapolikubali neno la Mungu wanachangamka wanapoliweka kando; na kukosa shauku na uhai wanapoliondokea. Kusema ukweli, nyinyi hamlithamini neno la Mungu hata kidogo, na kamwe hamyaoni maneno kutoka kinywa Chake Mwenyewe sasa kama hazina. Nyinyi huwa na wasiwasi tu mnapolisoma neno Lake, na kuhisi kuchoka mnapolikariri, na inapofika kuliweka neno la Mungu katika matendo, ni kama kujaribu kuzungusha mkono wa pampu ya kisima kwa kuuvuta na unywele kutoka katika mkia wa farasi—haijalishi jinsi utakavyojaribu, huwezi tu kutia nguvu ya kutosha. Nyinyi daima huwa mnachangamka mnaposoma neno la Mungu, lakini mnasahau mnapolitenda. Kwa hakika, maneno haya si lazima yazungumzwe kwa jitihada sana na kurudiwa kwa uvumilivu sana; lakini ukweli kwamba watu husikiliza tu bila kutia neno la Mungu katika vitendo umekuwa kizuizi kwa kazi Yake. Mimi siwezi kukosa kulitaja jambo hili, Mimi siwezi kukosa kulizungumzia. Mimi ninalazimika kufanya hivyo; siyo kwamba Mimi hufurahia kufunua udhaifu wa wengine. Mnafikiri kwamba matendo yenu kadiri yanatosha—kwamba wakati ambapo ufunuo uko kileleni, kuingia kwenu pia kumefikia kilele chake? Je, ni jambo rahisi sana hivyo? Kamwe hamchunguzi msingi ambao hatimaye hujenga uzoefu wenu! Kwa wakati huu, mikusanyiko yenu haiwezi kuitwa maisha yanayofaa ya kanisa hata kidogo, wala haijumuishi maisha yanayofaa ya kiroho kamwe. Ni mkusanyiko tu wa kundi la watu ambao hufurahia kuzungumza na kuimba. Kusema kweli, hakuna uhalisi mwingi ndani yake. Kueleza bayana, kama hutendi ukweli, uhalisi uko wapi? Je, huko siko kujigamba kusema kwamba una uhalisi? Wale ambao daima hufanya kazi ni wenye majivuno na wanaojipenda, wakati ambapo wale ambao hutii daima hutulia na kuinamisha vichwa vyao, bila nafasi yoyote ya kujifunza. Watu ambao hufanya kazi huwa hawafanyi chochote ila kuzungumza, wakizidi na mazungumzo yao yenye kuvutia, na wafuasi husikiliza tu. Hakuna mabadiliko ya kuzungumzia; Hizi zote ni njia za zamani tu! Leo, kuweza kwako kunyenyekea na kutohubutu kuingilia au kutenda jinsi unavyotaka ni kutokana na kuwasili kwa amri za kiutawala za Mungu; siyo mabadiliko uliyoyapata kupitia uzoefu. Ukweli kwamba huthubutu tena kufanya mambo fulani ambayo yanakiuka amri za kiutawala leo ni kwa sababu kazi ya Mungu ya maneno imekuwa na matokeo dhahiri na imewashinda watu. Acha Nimuulize mtu mmoja: Ni kiasi kipi cha mafanikio yako leo kilichopatikana kwa jasho la jitihada yako mwenyewe? Ni kiasi kipi ulichoambiwa moja kwa moja na Mungu? Ungejibu vipi? Je, ungepigwa na bumbuwazi na kutoweza kunena? Ni kwa nini wengine wanaweza kuzungumza juu ya uzoefu wao mwingi halisi ili kukuruzuku, wakati ambapo unafurahia tu chakula ambacho wengine wamepika? Je, huoni haya? Mnaweza kutekeleza uchunguzi wa kutafuta ukweli,

mkiwachunguza wale ambao kwa kulinganisha ni wazuri: Unaelewa ukweli kiasi kipi? Je, ni kiasi kipi ambacho wewe hatimaye huweka katika vitendo? Ni nani unayempenda zaidi, Mungu au wewe mwenyewe? Je, wewe hutoa mara nyingi zaidi, au hupokea mara nyingi zaidi? Je, ni mara ngapi umetelekeza nafsi yako ya zamani na kuyaridhisha mapenzi ya Mungu wakati lengo lako lilikuwa lenye kosa? Maswali haya machache tu yatawakanganya watu wengi. Kwa watu wengi, hata wakitambua kuwa nia yao si sahihi, bado wao hufanya makosa makusudi, nao hata hawajakaribia kuikana miili yao wenyewe. Watu wengi huruhusu dhambi kuenea kote ndani yao, wakiruhusu dhambi kuongoza kila tendo lao. Hawawezi kushinda dhambi zao, na wao huendelea kuishi katika dhambi. Baada ya kufika katika hatua hii ya sasa, ni nani asiyejua ni matendo mangapi mabaya ambayo ameyafanya? Ukisema kwamba hujui, basi unasema uongo kabisa. Kusema ukweli, yote ni kutotaka kutelekeza nafsi yako ya zamani. Je, kuna maana gani ya kusema “maneno ya dhati” yaliyo mengi sana ya kutubu ambayo ni bure? Je, hili linakusaidia kukua katika maisha yako? Inaweza kusemwa kwamba kujijua ni kazi yako ya kudumu. Mimi huwakamilisha watu kupitia utii wao na kutenda kwao maneno ya Mungu. Ukivaa tu neno la Mungu jinsi ambavyo ungevaa nguo zako, ili kuwa tu nadhifu na kupendeza, je, hujidanganyi mwenyewe na kuwadanganya wengine? Ikiwa yote uliyo nayo ni mazungumzo na kamwe huyaweki katika matendo, ni kitu gani utakachokipata?

Watu wengi wanaweza kuzungumza kidogo juu ya matendo na wanaweza kuzungumza kuhusu fikira zao za kibinafsi, lakini mengi ya hayo ni mwanga kutoka kwa maneno ya wengine. Hayajumuishi chochote kutoka kwa matendo yao binafsi hata kidogo, wala kujumuisha kile wanachokiona kutokana na uzoefu wao. Nimechambua suala hili mapema; usifikiri kwamba Sijui chochote. Wewe ni tishio la bure tu, lakini unazungumza juu ya kumshinda Shetani, juu ya kutoa ushuhuda wa ushindi, na kuishi kwa kudhihirisha mfano wa Mungu? Huu wote ni upuuzi! Je, unadhani kwamba maneno yote ambayo Mungu amenena leo ni ya wewe kupendezwa nayo? Kinywa chako hunena juu ya kutelekeza nafsi yako ya zamani na kuweka ukweli katika matendo, lakini mikono yako inafanya vitendo vingine na moyo wako unapanga hila zingine—wewe ni mtu wa aina gani? Kwa nini moyo wako na mikono yako si kitu kimoja? Kuhubiri kwingi sana kumekuwa maneno matupu; si hili ni jambo la kuvunja moyo? Ikiwa huwezi kuweka neno la Mungu katika matendo, inathibitisha kuwa bado hujaingia katika njia ambayo Roho Mtakatifu hufanya kazi, bado hujapata kuwa na kazi ya Roho Mtakatifu ndani yako, na bado hujapata mwongozo Wake. Ukisema kuwa unaweza tu kuelewa neno la Mungu lakini huwezi kuliweka katika matendo, basi wewe ni mtu asiyependa ukweli. Mungu haji kumwokoza mtu wa aina hii. Yesu alipatwa na maumivu makubwa wakati Aliposulubiwa ili kuwaokoa wenye dhambi, kuwaokoa maskini, na kuwaokoa wale watu wote wanyenyekevu. Kusulubiwa Kwake kulitumika kama sadaka ya dhambi. Ikiwa huwezi kutenda neno la Mungu, basi ni heri

uondoke haraka iwezekanavyo; usikawie katika nyumba ya Mungu kama mdoezi. Watu wengi hata huona vigumu kujizuia kufanya mambo ambayo humpinga Mungu kwa dhahiri. Je, si wanaalika kifo? Wanawezaje kuzungumza juu ya kuingia katika ufalme wa Mungu? Je, wataweza kuwa na ujasiri wa kuuona uso wa Mungu? Kula chakula ambacho Mungu hukupa, kufanya mambo ya uhalifu ambayo humpinga Mungu, kuwa mwenye nia mbaya, mwenye kudhuru kwa siri, na mwenye kufanya hila, hata wakati ambapo Mungu anakuruhusu ufurahie baraka ambazo Yeye amekupa—je, huzihisi zikiichoma mikono yako unapozipokea? Je, huhisi aibu? Baada ya kufanya kitu kinachompinga Mungu, baada ya kufanya hila ili “kuwa laghai,” je, huhisi hofu? Kama huhisi chochote, unawezaje kuzungumza juu ya wakati wowote ujao? Tayari kulikuwa hakuna wakati ujao kwako zamani za kale, kwa hiyo ni matarajio yapi makubwa zaidi unayoweza kuwa nayo bado? Ukisema kitu bila haya lakini huhisi lawama, na moyo wako hauna ufahamu, basi haimaanishi kwamba tayari umeachwa na Mungu? Kuzungumza na kutenda kwa kujiachilia na bila kuzuiwa kumekuwa asili yako; je, unawezaje kukamilishwa na Mungu hivi? Je, unaweza kutembea ulimwenguni kote? Ni nani anayeweza kushawishiwa na wewe? Wale ambao wanaijua asili yako ya kweli watakaa mbali nawe. Je, si hii ni adhabu ya Mungu? Kwa jumla, ikiwa kuna mazungumzo tu bila matendo, hakuna ukuaji. Ingawa Roho Mtakatifu anaweza kuwa akifanya kazi ndani yako unapozungumza, kama hutendi, Roho Mtakatifu ataacha kufanya kazi. Ukizidi kuendelea kwa njia hii, kunawezaje kuwa na majadiliano yoyote ya wakati ujao au kutoa nafsi yako yote kwa kazi ya Mungu? Unaweza tu kuzungumza juu ya kutoa nafsi yako yote, lakini hujampa Mungu upendo wako wa kweli. Yote Anayopata kutoka kwako ni upendo wa maneno tu; Yeye hapewi kusudi lako la kutenda ukweli. Je, hiki kinaweza kuwa ndicho kimo chako halisi? Ikiwa utaendelea kwa jinsi hii, utakamilishwa na Mungu lini? Je, huhisi wasiwasi juu ya kesho yako ya giza na majonzi? Je, huhisi kwamba Mungu amepoteza tumaini kwako? Je, hujui kwamba Mungu anatamani kuwakamilisha watu wengi zaidi na wapya zaidi? Je, vitu vya zamani vinaweza kudumu? Wewe huyazingatii maneno ya Mungu leo: Je, unasubiri kesho?

Kile Ambacho Mchungaji wa Kutosha Anapaswa Kujiandaa Nacho

Lazima uwe na ufahamu wa hali nyingi ambazo watu watakuwa ndani wakati Roho Mtakatifu anafanya kazi juu yao. Hasa, wale wanaofanya kazi kwa namna sawa kumtumikia Mungu lazima wawe na ufahamu bora zaidi wa hali nyingi zinazoletwa na kazi ambayo Roho Mtakatifu hutekeleza kwa wanadamu. Ikiwa unasema tu kuhusu uzoefu mwingi na njia nyingi za kuingia ndani, inaonyesha kwamba uzoefu wako unaegemea upande mmoja sana. Bila kujua hali yako ya kweli au kufahamu kanuni za ukweli, haiwezekani kufikia mabadiliko katika tabia. Bila

kujua kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu au kuelewa matokeo yatokayo hapo, itakuwa vigumu kutambua kazi ya pepo wabaya. Lazima ufunue kazi ya pepo wabaya na mawazo ya wanadamu na uende moja kwa moja kwenye kiini cha suala hili; lazima pia uonyeshe mikengeuko mingi katika utendaji wa watu au matatizo katika kumwamini Mungu ili waweze kuyatambua. Kwa kiwango cha kidogo sana, lazima usiwafanye kuhisi hasi au wasiojishughulisha. Hata hivyo, lazima uelewe shida ambazo zipo kwa watu wengi bila upendeleo, hupaswi kuwa bila busara au “ujaribu kumfunza nguruwe kuimba”; hiyo ni tabia ya upumbavu. Ili kutatua matatizo mengi ya wanadamu, lazima uelewe elimumwendo ya kazi ya Roho Mtakatifu, lazima uelewe jinsi Roho Mtakatifu anavyotekeleza kazi kwa watu tofauti, lazima uelewe matatizo ya wanadamu, upungufu wa wanadamu, ubaini masuala muhimu ya shida, na kufikia chanzo cha tatizo, bila mkengeuko au makosa. Ni mtu wa aina hii tu ndiye aliyestahiki kuratibu kumhudumia Mungu.

Bila kujali kama unaweza kuelewa masuala muhimu na kuona kwa dhahiri mambo mengi hutegemea uzoefu wako binafsi. Namna ambavyo unapitia ndiyo pia namna ambavyo unaowaongoza wengine. Ikiwa unaelewa barua na mafundisho, basi unawaongoza wengine kuelewa barua na mafundisho. Njia ambayo unapitia ukweli wa maneno ya Mungu ndiyo njia ambayo unawaongoza wengine kuingia katika ukweli wa maneno ya Mungu. Ikiwa unaweza kuelewa ukweli mwingi na kuona kwa dhahiri mambo mengi katika maneno ya Mungu, basi unaweza kuwaongoza wengine kuelewa ukweli mwingi, na wale unaowaongoza watakuwa na ufahamu wa wazi wa maono. Ukilenga kushika hisia zisizo za kawaida, basi wale unaowaongoza pia watalenga hisia zisizo za kawaida. Ikiwa unapuuza matendo na kusisitiza kuzungumza, basi wale unaowaongoza pia watazingatia kuzungumza, bila utekelezaji wowote, bila mbadiliko wowote katika tabia zao, na watakuwa tu na shauku kwa nje, bila kutenda ukweli wowote. Wanadamu wote huwatolea wengine kile walicho nacho wenyewe. Aina ya mtu huamua njia ambayo anawaongoza wengine kuingia, na aina ya mtu huamua aina ya watu anaowaongoza. Ili kuwa wa kufaa kwa matumizi ya Mungu, hamhitaji tu kuwa na matarajio, lakini mnahitaji pia nuru nyingi kutoka kwa Mungu, mwongozo kutoka kwa maneno ya Mungu, kushughulikiwa na Mungu, na usafishaji wa maneno Yake. Hili likiwa msingi, katika nyakati za kawaida, mnapaswa kutilia maanani uchunguzi, mawazo, kutafakari na hitimisho, na mjishughulishe na uingiaji au uondolewaji inavyopasa. Hizi zote ni njia za kuingia kwenu katika uhalisi na zote ni za msingi— hii ndiyo njia ambayo Mungu hufanya kazi. Ikiwa unapaswa kuingia katika njia hii ambayo Mungu hufanya kazi, basi utakuwa na fursa ya kukamilishwa na Mungu kila siku. Na wakati wowote, bila kujali kama ni mazingira magumu au mazingira mazuri, kama unajaribiwa au unashawishiwa, kama unafanya kazi au la, kama unaishi maisha kama mtu binafsi au kwa pamoja, utapata fursa za kukamilishwa na Mungu kila wakati, bila kukosa hata moja yao. Utakuwa na uwezo wa kugundua zote, na kwa njia hii utakuwa umepata siri ya kupitia maneno

ya Mungu.

Kuhusu Uzoefu

Katika uzoefu wote wa Petro, alikumbana na mamia ya majaribio. Ingawa watu wa leo wanafahamu neno “jaribio,” wao huchanganyikiwa kuhusiana na maana yake ya kweli na hali. Mungu hutuliza azimio la watu, husafisha imani yao, na hukamilisha kila sehemu yao—na hii hufanikishwa kimsingi kupitia majaribio, ambayo pia ni kazi ya Roho Mtakatifu iliyofichwa. Inaonekana kama kwamba Mungu amewaacha watu, na kwa hivyo wasipokuwa waangalifu, watayaona majaribio haya kama majaribu ya Shetani. Kwa kweli, majaribio mengi yanaweza kufikiriwa kuwa majaribu, na hii ni kanuni na sheria ambazo Mungu hufanya kazi kupitia kwazo. Watu wakiishi mbele ya Mungu kwa kweli, wataona vitu vile kama majaribio kutoka kwa Mungu, na hawataviruhusu viponyoke. Mtu akisema kwamba kwa sababu Mungu yu pamoja naye Shetani hakika hatamwendea, hii siyo sahihi kabisa; je, basi inaweza kuelezwa vipi kwamba Yesu alikabiliwa na majaribu baada ya Yeye kufunga jangwani kwa siku arobaini? Kwa hivyo watu wakirekebisha maoni yao juu ya imani katika Mungu, wataona mambo mengi kwa uwazi zaidi, na ufahamu wao hautakuwa wa upogoupogo na wa uongo. Ikiwa mtu kwa kweli ameamua kukamilishwa na Mungu, anapaswa kuyakabili masuala yanayomkabili toka kwa mitazamo mingi tofauti, bila kuyumbayumba upande wa kushoto wala kulia. Ikiwa huna maarifa ya kazi ya Mungu, hutajua jinsi ya kushirikiana na Mungu. Ikiwa hujui kanuni za kazi ya Mungu, na hujui jinsi Shetani anavyofanya kazi kwa mwanadamu, hutakuwa na njia ya kutenda. Ufuatiliaji wenye ari pekee hautakuruhusu ufikie matokeo yanayohitajiwa na Mungu. Mbinu kama hiyo ya kupitia ni sawa na ile ya Lawrence: kutotofautisha hali yoyote kabisa na kulisitiza uzoefu tu, kutojua kabisa kazi ya Shetani ni nini, kutojua kazi ya Roho Mtakatifu ni nini, jinsi mwanadamu alivyo bila kuwepo kwa Mungu, na ni watu wa aina gani ambao Mungu anataka kuwakamilisha. Ni kanuni gani zinapaswa kukubaliwa wakati wa kushughulikia aina tofauti za watu, jinsi ya kuelewa vizuri mapenzi ya Mungu sasa, jinsi ya kujua tabia ya Mungu, na ni kwa watu, mazingira, na enzi gani ndiyo huruma, uadhama, na haki ya Mungu huelekezwa—hana utambuzi wowote kuhusu yoyote kati ya haya. Ikiwa watu hawana maono mengi kama msingi wa uzoefu wao, basi uzima haupo, sembuse uzoefu; wanaweza kuendelea kutii na kuvumilia kila kitu kwa upumbavu. Watu kama hawa ni vigumu sana kuwakamilisha. Inaweza kusemwa kuwa ikiwa huna maono yoyote yaliyotajwa hapo juu, hili ni thibitisho tosha kwamba wewe ni mpumbavu, wewe ni kama nguzo ya chumvi ambayo husimama daima katika Israeli. Watu kama hawa ni bure, vinyangarika! Watu wengine hutii kila mara bila kufikiri, wao daima hujitambua na hutumia njia zao wenyewe za kutenda wanaposhughulikia masuala mapya, au wanatumia “hekima” kushughulikia mambo madogo na yasiyofaa kutajwa. Watu kama hao hawana utambuzi, ni kama kwamba asili yao ni kukubali kuonewa bila kulalamika, na wao daima huwa

vilevile, hawabadiliki kamwe. Watu kama hawa ni wapumbavu ambao hawana utambuzi hata kidogo. Kamwe hawajaribu kulinganisha matendo kwa hali au watu tofauti. Watu kama hawa hawana uzoefu. Nimewaona watu fulani ambao hushughulika sana katika ujuzi wao wenyewe kiasi kwamba wanapokabiliwa na watu walio na kazi ya pepo waovu, huinamisha vichwa vyao na kukiri dhambi zao, bila kuthubutu kusimama na kuwashutumu. Na wanapokabiliwa na kazi dhahiri ya Roho Mtakatifu, hawathubutu kutii. Wanaamini kwamba pepo hawa waovu pia wako mikononi mwa Mungu, na hawana ujasiri hata kidogo wa kusimama na kuwapinga. Watu kama hawa wanamwaibisha Mungu, na hawawezi kabisa kubeba mzigo mzito kwa ajili ya Mungu. Wapumbavu kama hawa hawaleti tofauti ya aina yoyote. Kwa hivyo, mbinu kama hiyo ya kupata uzoefu, inapaswa kusafishwa, kwani haiwezi kuthibitishwa machoni pa Mungu.

Hakika Mungu hufanya kazi nyingi kwa watu, wakati mwingine kuwajaribu, wakati mwingine kusababisha mazingira ya kuwatuliza, na wakati mwingine kuzungumza maneno ili kuwaongoza na kurekebisha upungufu wao. Wakati mwingine Roho Mtakatifu huwaongoza watu kwenye mazingira yaliyotayarishwa na Mungu kwao ili wagundue mambo mengi ambayo hawana. Kupitia kile ambacho watu husema na kufanya, jinsi ambavyo watu huwatendea wengine na kuvishughulikia vitu, bila wao kujua, Roho Mtakatifu huwapa nuru kuhusu vitu vingi ambavyo hawakuvielewa hapo zamani, Akiwaruhusu waone mambo mengi na watu kwa uwazi zaidi, Akiwaruhusu wabaini mengi kuhusu yale ambayo hawakuyajua hapo zamani. Unapojishughulisha na ulimwengu, unanza kutambua mambo ya ulimwengu hatua kwa hatua, na kabla ya kufikia mwisho wako, unaweza kufikia uamuzi: “Ni vigumu kweli kuwa mtu.” Ukitumia muda kiasi kupata uzoefu mbele ya Mungu, na kuja kuelewa kazi ya Mungu na tabia Yake, utapata umaizi zaidi bila kufahamu, na kimo chako kitakua polepole. Utaelewa mambo mengi ya kiroho vizuri zaidi, na utakuwa na hakika zaidi kuhusu kazi ya Mungu hasa. Utakubali maneno ya Mungu, kazi ya Mungu, kila tendo la Mungu, tabia ya Mungu, na kile Mungu alichona kile Anacho kama uzima wako mwenyewe. Ikiwa yote unayofanya ni kuzurura ulimwenguni, mabawa yako yatakua magumu zaidi, na upinzani wako dhidi ya Mungu utakuwa mkubwa zaidi; hivyo basi Mungu anawezaje kukutumia? Kwa sababu kuna “kwa maoni yangu” kwa wingi sana ndani yako, Mungu hawezi kukutumia. Kadiri unavyozidi kuwa mbele ya Mungu, ndivyo utakavyokuwa na uzoefu zaidi. Ikiwa wewe bado unaishi ulimwenguni kama mnyama, kinywa chako kikitangaza imani katika Mungu lakini moyo wako ukiwa mahali pengine, na kama bado unazichunguza falsafa za kidunia za kuishi, basi si kazi zako zote za awali zitakuwa bure? Kwa hivyo, kadiri watu wanavyozidi kuwa mbele ya Mungu, ndivyo inavyokuwa rahisi zaidi kwao kukamilishwa na Mungu. Hii ndiyo njia ambayo kwayo Roho Mtakatifu hufanya kazi Yake. Usipoelewa hili, haitawezekana wewe kuingia kwenye njia sahihi, na kukamilishwa na Mungu hakutawezekana. Hutaweza kuwa na maisha ya kawaida ya kiroho, itakuwa kama kwamba wewe

ni mlemavu, utakuwa tu na bidii yako na bila kazi yoyote ya Mungu. Je, si hili ni kosa katika uzoefu wako? Si lazima uombe ili uwe mbele ya Mungu; wakati mwingine ni katika kufikiri kwako juu ya Mungu au kutafakari kazi Yake, wakati mwingine katika kushughulikia kwako suala fulani, na wakati mwingine kwa njia ya kufichuliwa kwako katika tukio, ndipo wewe huja mbele ya Mungu. Watu wengi husema, “Je, siko mbele ya Mungu, kwa kuwa mimi mara nyingi huomba?” Watu wengi huomba bila kukoma “mbele ya Mungu.” Sala zinaweza kuwa daima kwenye midomo yao, lakini hawaishi kwa kweli mbele ya Mungu. Hii ndiyo njia pekee ambayo watu hao wanaweza kudumisha hali zao mbele ya Mungu; hawawezi kabisa kutumia mioyo yao kushirikiana na Mungu wakati wote, wala hawawezi kuja mbele ya Mungu kwa njia ya kupata uzoefu, iwe kwa njia ya kuwaza, kutafakari kwa kimya, au kutumia mawazo yao kushirikiana na Mungu ndani ya mioyo yao kwa kuzingatia mzigo wa Mungu. Wao hutoa tu sala kwa Mungu mbinguni wakitumia vinywa vyao. Mioyo ya watu wengi haina Mungu, Mungu yuko pale tu wakati ambapo wanamkaribia; mara nyingi, Mungu hayupo kabisa. Je, si hili ni dhihirisho la kutokuwa na Mungu katika moyo wa mtu? Kama kweli wangukuwa na Mungu mioyoni mwao, je, wangepanya mambo ambayo wezi na wanyama hufanya? Ikiwa mtu anamcha Mungu kwa kweli, ataleta moyo wake wa kweli kuwa karibu na Mungu, na mawazo na dhana zao daima zitamilikiwa na maneno ya Mungu. Hatafanya makosa katika usemi au vitendo, na hatafanya chochote kinachompinga Mungu waziwazi. Hicho ndicho kiwango cha kuwa muumini.

Amri za Enzi Mpya

Katika kupitia kazi ya Mungu, ninyi lazima msome maneno ya Mungu kwa makini na mjiandae na ukweli. Lakini kuhusu kile mnachotaka kufanya au jinsi mnavyotaka kukifanya, hakuna haja ya maombi au dua yenu ya dhati, na kwa kweli mambo haya hayana maana. Ilhali kwa sasa, shida zinazowakabili hivi sasa ni kwamba hamjui jinsi ya kupitia kazi ya Mungu, na kwamba kuna ubaridi mwingi ndani mwenu. Mnajua mafundisho mengi, lakini hamna uhalisi mwingi. Je, hii si ishara ya makosa? Makosa mengi yanaonekana ndani yenu, kundi hili. Hivi leo, hamna uwezo wa kutimiza majaribu kama vile “watendaji huduma,” na hamwezi kutafakari au kutimiza majaribu na usafishaji mwingine unaohusiana na maneno ya Mungu. Lazima mzingatie mambo mengi ambayo mnapaswa kuweka katika matendo. Ambayo ni kusema kuwa watu lazima wafuate majukumu mengi wanayostahili kuyatekeleza. Hili ndilo watu wanalopaswa kufuata, na wanalostahili kufanya. Mruhusu Roho Mtakatifu afanye linalostahili kufanywa na Roho Mtakatifu; mwanadamu hawezi kulichangia lolote. Mwanadamu sharti ashike yale ambayo lazima yatendwe na mwanadamu, ambayo hayana uhusiano na Roho Mtakatifu. Si lolote bali lile ambalo lazima litendwe na mwanadamu, na lazima lifuatwe kama amri, kama ufuasi wa sheria za Agano la Kale. Ingawa sasa si Enzi ya Sheria, bado kuna maneno mengi yanayolingana na Enzi ya Sheria ambayo yanahitaji kufuatwa, na hayatendwi tu kwa kutegemea

kuguswa na Roho Mtakatifu, lakini ni yale yanayostahili kufuatwa na wanadamu. Kwa mfano: Hupaswi kuihukumu kazi ya Mungu wa vitendo. Hupaswi kumpinga mtu anayeshuhudiwa na Mungu. Mbele za Mungu, utahifadhi nafasi yako, na hutakuwa mwovu. Matamshi yako yanapaswa yawe wastani, na maneno yako na matendo yako yanapaswa kufuata mpangilio wa mwanadamu aliyeshuhudiwa na Mungu. Unapaswa kuheshimu ushuhuda wa Mungu. Usipuuze kazi ya Mungu wala maneno kutoka kinywa chake. Usiige sauti na malengo ya matamshi ya Mungu. Kwa nje, usifanye lolote linalodhihirisha kumpinga mtu anayeshuhudiwa na Mungu. Na mengineyo. Haya ndiyo yanayopaswa kufuatwa na kila mmoja. Katika kila enzi, Mungu hutaja amri nyingi zinazoambatana na amri na zinazopaswa kufuatwa na mwanadamu. Kupitia hili, anazuia tabia ya mwanadamu, na kugundua ukweli wake. Tazama maneno “Onyesha heshima kwa baba na mama yako” kutoka kwa nyakati za Agano la Kale, kwa mfano. Maneno haya hayatumiki hivi leo; wakati huo, yalizuia tabia zingine za mwanadamu tu, yalitumika kuonyesha uaminifu wa imani ya mwanadamu kwa Mungu, na yalikuwa alama ya wale waliomwamini Mungu. Ingawa sasa ni Enzi ya Ufalme, bado kuna amri nyingi ambazo mwanadamu lazima azifuate. Amri za kale hazitumiki; leo, kuna mazoea mengi, mwafaka kwa mwanadamu kutekeleza, na ambayo ni muhimu. Hayahusiani na kazi ya Roho Mtakatifu na lazima yatendwe na mwanadamu.

Katika Enzi ya Neema, mazoea mengi ya Enzi ya Sheria yaliondolewa kwa sababu sheria hizi hazikufaa hasa kazi ya wakati huo. Baada ya kuondolewa, mazoea mengi yaliwekwa ambayo yalifaa enzi hiyo, na ambayo yamekuwa amri nyingi za sasa. Mungu wa leo alipokuja, kanuni hizi zilitupiliwa mbali, na hazikuhitajika kufuatwa tena, na mazoea mengi ambayo yalifaa kazi ya wakati huu yakawekwa. Leo, mazoea haya si kanuni, lakini ili kuwa na athari; ni mazuri kwa ajili ya leo—na kesho, pengine, yatakuwa kanuni. Kwa ujumla, unafaa kufuata yale ambayo yatafanikisha kazi ya leo. Usizingatie kesho: Yanayofanywa leo ni kwa ajili ya leo. Pengine kesho kutakuwa na mazoea mazuri ambayo utahitajika kutekeleza—lakini usizingatie hayo sana, yafuate yanayofaa kufuatwa leo ili uepuke kumpinga Mungu. Leo, hakuna lolote muhimu analopaswa kufuata mwanadamu zaidi ya yafuatayo: Usijaribu kumbembeleza Mungu anayesimama mbele ya macho yako, au kumficha jambo lolote. Usizungumze uchafu ama matamshi ya kiburi mbele ya Mungu aliye mbele yako. Usimdanganye Mungu mbele ya macho yako kwa maneno mazuri wala kwa maneno ya kuridhisha ili uweze kujipatia uaminifu Wake. Usitende bila heshima mbele za Mungu. Tii yote yatokayo kinywani mwa Mungu, wala usikatae, usipinge, ama kusaili maneno Yake. Usitafsiri unavyoona kuwa sawa, maneno yanayonenwa kutoka kinywani mwa Mungu. Chunga ulimi wako ili usikutie katika mtego wa hila danganyifu za yule mwovu. Unapaswa kulinda nyayo zako ili kuepuka kupita mipaka uliyowekewa na Mungu. Kufanya hivyo kutakufanya uzungumze maneno ya majivuno na yenye fahari kuu

kulingana na mtazamo wa Mungu, na hivyo kufanya uchukiwe na Mungu. Usieneze maneno kutoka kinywa cha Mungu ovyo ovyo, usije ukadhihakiwa na wengine na kufanywa kuwa mjinga na mapepo. Tii kazi yote ya Mungu wa leo. Hata ikiwa hauifahamu, usiihukumu; unachoweza kufanya ni kutafuta na kushiriki. Hakuna mtu atapatendea dhambi mahali pa Mungu pa asili. Huwezi kufanya lolote ila kumhudumia Mungu wa leo kwa mtazamo wa mwanadamu. Huwezi kumfunza Mungu wa leo kwa mtazamo wa mwanadamu—kufanya hivyo ni kupotoka. Hakuna anayeweza kusimama kwa niaba ya mtu aliyeshuhudiwa na Mungu; katika maneno yako, matendo, na mawazo yako ya ndani, unasimama katika nafasi ya mwanadamu. Hili ni la kufuatwa, ni wajibu wa mwanadamu, hakuna anayeweza kulibadilisha, na kufanya hivyo ni ukiukaji wa amri za utawala. Inapaswa kukumbukwa na kila mtu.

Muda mrefu ambao Mungu ametumia kuzungumza na kutamka kumemfanya mwanadamu kufikiria kusoma na kukariri maneno ya Mungu kuwa ndio wajibu wake wa kimsingi. Hakuna anayezingatia kutenda, na hata yale mnayopaswa kufuata hamyafuati, kwa hivyo hili limeleta ugumu na matatizo mengi kwa huduma yenu. Ikiwa, kabla ya kutenda maneno ya Mungu, hujayafuata yale unayopaswa kuyafuata, basi wewe ni mmoja wa wale wanaochukiwa na kukataliwa na Mungu. Kwa kufuata matendo haya, unapaswa kuwa na bidii na uaminifu. Hufai kuyachukua kuwa kama minyororo, ila uyafuate kama amri. Leo, hupaswi kuzingatia athari ambazo zinatarajiwa kufikiwa; kwa ufupi, hivi ndivyo Roho Mtakatifu anavyofanya kazi, na yeyote atakayefanya kosa lazima aadhibiwe. Roho Mtakatifu hana hisia, na hazingatii ufahamu wako wa sasa. Ukimkosea Mungu leo, basi Atakuadhibu. Ukimkosea ndani ya wigo wa mamlaka Yake, basi Hatakuachilia bure. Hajali jinsi gani ulivyo makini katika kufuata maneno ya Yesu. Ukikiuka amri za Mungu za leo, Atakuadhibu; Atakushutumu hadi kifo. Je, itakubalika vipi kwako wewe kutozifuata? Lazima ufuate—hata kama itamaanisha kupitia uchungu mdogo! Bila kujali ni dini, kundi, taifa, ama dhehebu gani, katika siku zijazo lazima yote yafuate mazoea haya. Hakuna yaliyosamehewa, na hakuna yatakayoachwa! Kwa sababu ndiyo yatakayotekelezwa na Roho Mtakatifu leo, na hayawezi kukosewa kwa wote. Ingawa si mambo makuu, lazima yatendwe na kila mtu, na ni amri zilizowekwa kwa mwanadamu na Yesu, aliyefufuka na kupaa mbinguni. Je, “Njia ... (7)” haisemi kuwa ufafanuzi wa Yesu, wa kama wewe ni mwenye haki au mwenye dhambi, ni kwa mujibu wa mtazamo wako kwa Mungu leo? Hakuna anayekubaliwa kupuuza suala hili. Katika Enzi ya Sheria, kizazi baada ya kizazi cha Mafarisayo kilimwamini Mungu, lakini kwa ujio wa Enzi ya Neema, hawakumfahamu Yesu, na walimpinga. Hivyo basi, yote waliyoyafanya yakawa hayana maana na yalikuwa bure na Mungu hakuyakubali. Ukiweza kuelewa hili basi hutakuwa mwepesi wa kutenda dhambi. Watu wengi, pengine, wamejipima dhidi ya Mungu. Je, kumpinga Mungu kuna ladha ipi, chungu au tamu? Unapaswa kuelewa hili—usijifanye kuwa hujui. Mioyoni mwao, pengine, wengine wamesalia

kutoshawishika. Bali Nakushauri, ulijaribu na kuona—hisi jinsi ladha yake ilivyo. Hili litawazuia wengi kuwa na shaka kulihusu siku zote. Watu wengi husoma maneno ya Mungu lakini wanampinga mioyoni mwao kwa siri. Baada ya kumpinga hivi, je, huhisi kama kisu kimepindwa moyoni mwako? Kama si utengano wa familia, basi ni usumbufu wa mwilini, ama mateso ya wana wa kiume na mabinti. Ingawa mwili wako umeepushwa na kifo, mkono wa Mungu kamwe hautakuacha. Je, unafikiri linaweza kuwa rahisi hivyo? Hasa, ni muhimu hata zaidi kwa wengi waliomkaribia Mungu kuzingatia hili. Muda unapoendelea, utalisahau, na, pasipo kujua, utaingia majaribuni, utaacha kujali kila kitu, na huu utakuwa mwanzo wako wa kutenda dhambi. Je, hili linaonekana duni kwako? Ikiwa utaweza kufanya hili vyema, basi una nafasi ya kufanywa mkamilifu—kupokea mwongozo kutoka kwa kinywa cha Mungu mwenyewe mbele za Mungu. Ikiwa wewe ni mzembe, itakuwa taabu kwako—utamwasi Mungu, maneno yako na matendo yatakuwa maovu, na punde au baadaye, utabebwa na dhoruba kubwa na mawimbi makuu. Kila mmoja wenu anapaswa kuzingatia amri hizi. Mkizikiuka, mtu aliyeshuhudiwa na Mungu anaweza akakosa kuwalaani, lakini Roho wa Mungu hajamalizana na wewe. Hatakuhurumia. Je, unadhania kwamba una uwezo wa kufanya makosa? Kwa hivyo, lolote Asemalo Mungu, lazima utie katika vitendo maneno Yake, na kuyafuata kwa njia zozote unazoweza. Hili si jambo rahisi!

Ufalme wa Milenia Umewasili

Je, mmeona kazi ambayo Mungu ataikamilisha katika kundi hili la watu? Mungu alisema, hata katika Ufalme wa Milenia watu ni lazima waendeleo kufuata matamshi Yake, na katika maisha ya baadaye, matamshi ya Mungu bado yatakuwa yanaongoza maisha ya mwanadamu moja kwa moja kwenda katika nchi ya Kanaani. Musa alipokuwa jangwani, Mungu alimwelekeza na kuzungumza naye moja kwa moja. Kutoka mbinguni Mungu alituma chakula, maji, na mana ili watu waweze kuvifurahia, na leo bado ni hivyo: Mungu mwenyewe ametuma vitu chini kwa ajili ya kula na kunywa ili watu wafurahi, na yeye mwenyewe ametuma laana ili kuwadhibu watu. Na hivyo kila hatua ya kazi Yake inafanywa na Mungu Mwenyewe. Leo, watu wanatamani utokeaji wa kweli, wanajaribu kuona ishara na maajabu, na kuna uwezekano mkubwa watu wa namna hiyo kutelekezwa, maana kazi ya Mungu inazidi kuwa halisi. Hakuna anayejua kwamba Mungu ameshuka kutoka mbinguni, bado hawajui kwamba Mungu ametuma chini chakula na maji ya kutia nguvu kutoka mbinguni, lakini Mungu kimsingi yupo, na mazingira mazuri ya Ufalme wa Milenia ambao watu wanaufikiria pia ni matamshi ya Mungu Mwenyewe. Huu ni ukweli, ni huu tu ndio unaotawala pamoja na Mungu duniani. Kutawala na Mungu duniani kunarejelea mwili. Kile ambacho si cha mwili hakipo duniani, na hivyo wale wote wanaojikita katika kusonga mbele katika mbingu ya tatu wanafanya hivyo bure. Siku moja, ambapo ulimwengu mzima utarudi kwa Mungu, kitovu cha kazi Yake katika ulimwengu wote kitafuata matamko ya Mungu; kwingineko watu watapiga simu, wengine watapanda ndege,

wengine watapanda boti na kupita baharini, na wengine watatumia leza kupokea matamshi ya Mungu. Kila mmoja atakuwa anatamani na mwenye shauku, wote watakuja karibu na Mungu, na kukusanyika kwa Mungu, na wote watamwabudu Mungu—na yote haya yatakuwa matendo ya Mungu. Kumbuka hili! Mungu hawezi kuanza tena kwingineko. Mungu atatimiza ukweli huu: Atawafanya watu wote ulimwengu mzima kuja mbele Yake, na kumwabudu Mungu duniani, na kazi Yake katika maeneo mengine itakoma, na watu watalazimishwa kutafuta njia ya kweli. Itakuwa kama Yusufu: Kila mtu alimwendea kwa ajili ya chakula, na kumsujudia, kwa sababu alikuwa na vyakula. Ili kuweza kuepuka njaa watu watalazimishwa kutafuta njia ya kweli. Jumuiya yote ya kidini itapitia njaa kubwa, na ni Mungu tu wa leo ndiye chemchemi ya maji ya uzima, akiwa na kisima chenye maji yasiyokauka kilichotolewa kwa ajili ya furaha ya mwanadamu, na watu watakuja na kumtegemea. Huo ndio utakuwa muda ambapo matendo ya Mungu yatafichuliwa, na Mungu atatukuzwa; watu wote katika ulimwengu wote watakuja na kumwabudu “mtu” asiyekuwa wa kawaida. Je, hii haitakuwa siku ya utukufu wa Mungu? Siku moja, wachungaji wa zamani watatuma ujumbe wakitafuta maji kutoka katika chemchemi za maji ya uzima. Watakuwa wazee, lakini watakuja kumwabudu mtu huyu ambaye walimdharau. Katika vinywa vyao watakiri na katika mioyo yao wataamini—je, hii si ishara na maajabu? Siku ambapo ufalme wote utafurahia ni siku ya utukufu wa Mungu, na mtu yeyote atakayewajia, na kupokea habari njema za Mungu atabarikiwa na Mungu, na nchi hizi na watu hawa watabarikiwa na kulindwa na Mungu. Mwelekeo wa maisha yajayo utakuwa hivi: Wale ambao watapata matamshi kutoka katika kinywa cha Mungu watakuwa na njia ya kutembea duniani, na wawe wafanya biashara au wanasayansi, au waelimishaji au wataalamu wa viwandani, wale ambao hawana maneno ya Mungu watakuwa na wakati mgumu wa kuchukua hata hatua moja, na watalazimishwa kutafuta njia ya kweli. Hiki ndicho kinamaanishwa na, “Ukiwa na ukweli utatembea ulimwengu mzima; bila ukweli, hutafika popote.” Ukweli ni huu: Mungu atatumia Njia (ikiwa na maana kwamba maneno Yake yote) kuuamuru ulimwengu wote na kumwongoza na kumshinda mwanadamu. Watu siku zote wanatarajia kuwa na mageuko makubwa katika namna ambayo Mungu anafanya kazi. Kuzungumza kwa wazi, ni kupitia maneno ndipo Mungu anawadhibiti watu, na unapaswa kufanya kile Anachokisema haijalishi kama unataka au hutaki; huu ni ukweli halisi, na unapaswa kutiiwa na watu wote, na hivyo haubadiliki, na kujulikana kwa wote.

Roho Mtakatifu anawapatia watu hisia. Baada ya kusoma maneno ya Mungu, katika mioyo yao wamesimama imara, na wana amani, wakati wale ambao hawapati maneno ya Mungu wanajihisi watupu. Hiyo ni nguvu ya maneno ya Mungu—watu wanapaswa kuyasoma, baada ya kuyasoma wananawirishwa, na hawawezi kufanya chochote bila hayo. Ni kama ambapo watu wanatumia afyuni: Inawapatia nguvu, na bila hiyo wanahisi nguvu yake ya kuvuta, na wanakosa

nguvu. Hayo ndiyo mazoea miongoni mwa watu leo. Kusoma maneno ya Mungu kunawapatia watu nguvu. Ikiwa hawayasomi, wanajiona hawana nguvu, lakini baada ya kuyasoma, wanainuka mara moja kutoka katika “kitanda cha mgonjwa.” Hii ni neno la Mungu kutawala duniani na Mungu kutawala ulimwenguni. Baadhi ya watu wanataka kuacha au wamechoshwa na kazi ya Mungu. Licha ya hayo, hawawezi kujitenganisha na maneno ya Mungu; bila kujali ni wadhaifu kiasi gani, bado ni lazima waishi kwa kutegemea maneno ya Mungu ili waishi, na haijalishi ni watu wa uasi kiasi gani, lakini bado hawathubutu kuacha maneno ya Mungu. Pale ambapo maneno ya Mungu yanaonyesha ukuu wao ndipo ambapo Mungu anatawala na kuchukua nguvu, na hivi ndivyo Mungu anavyofanya kazi. Hata hivyo, hii ndiyo njia ambayo kwayo Mungu anafanya kazi, na hakuna anayeweza kuiacha. Maneno ya Mungu yataenea katika nyumba zisizohesabika, yatafahamika kwa wote, na wakati huo tu ndipo kazi yake itaenea ulimwenguni kote. Ambapo ni sawa na kusema, ikiwa kazi ya Mungu itaenea ulimwenguni kote, basi maneno Yake ni lazima yaenee. Katika siku ya utukufu wa Mungu, maneno ya Mungu yataonesha nguvu yake na mamlaka. Kila neno Lake kuanzia wakati huo hadi leo litatimizwa na kuwa la kweli. Kwa njia hii, utukufu utakuwa wa Mungu duniani—ambavyo ni sawa na kusema, kazi yake itatawala duniani. Wote ambao ni waovu wataadibiwa na maneno katika kinywa cha Mungu, wale wote ambao ni wa haki watabarikiwa na maneno katika kinywa Chake, na wote watathibitishwa na kukamilishwa na maneno katika kinywa Chake. Wala hataonyesha ishara zozote na maajabu; yote yatakamilishwa na maneno Yake, na maneno Yake yatazalisha ukweli. Kila mtu duniani atasherehekea maneno ya Mungu, ama ni watu wazima au watoto, wanaume, wanawake, wazee, au vijana, watu wote watajinyenyekeza katika maneno ya Mungu. Maneno ya Mungu yaonekana katika mwili, yakiwaruhusu watu kuyaona duniani, waziwazi na kufanana na kiumbe chenye uhai. Hii ndiyo maana ya Neno kufanyika mwili. Mungu amekuja duniani kwa lengo la kukamilisha ukweli wa “Neno kufanyika mwili,” ni sawa na kusema, Amekuja ili kwamba maneno Yake yaweze kutolewa kutoka katika mwili (sio kama wakati wa Musa katika Agano la Kale, ambapo Mungu alizungumza moja kwa moja kutoka mbinguni). Baada ya hapo, kila neno Lake litatimizwa wakati wa Enzi ya Ufalme wa Milenia, zitakuwa ni kweli ambazo zitaonekana katika macho ya watu, na watu watazitamama kwa kutumia macho bila tofauti hata kidogo. Hii ndiyo maana kuu ya Mungu kupata mwili. Ni sawa na kusema, kazi ya Roho imetimizwa kupitia mwili, na kupitia maneno. Hii ndiyo maana ya kweli ya “Neno kufanyika mwili” na “Neno Laonekana katika mwili.” Ni Mungu pekee ndiye anayeweza kuzungumza mapenzi ya Roho, na ni Mungu pekee katika mwili ndiye anayeweza kuzungumza kwa niaba ya Roho; maneno ya Mungu yamewekwa wazi katika Mungu kupata mwili, na kila mtu anaongozwa nayo. Hakuna aliyeachwa, wote wanakuwa ndani ya mawanda haya. Ni kutoka tu katika matamshi haya ndipo watu wanaweza kujua; wale ambao hawatapata njia hii wanaota ndoto za mchana ikiwa wanadhani wanaweza kupata matamshi kutoka mbinguni. Hayo ndiyo

mamlaka yaliyooneshwa katika mwili wa Mungu uliopata mwili: kuwafanya wote kuamini. Hata wataalamu wa kuheshimiwa sana na wachungaji hawawezi kuzungumza maneno haya. Wote ni lazima wajinyenyekeze chini yao, na hakuna anayeweza kuanza mwanzo mpya. Mungu atatumia maneno kuushinda ulimwengu. Atafanya hivi si kwa kupata kwake mwili, lakini kwa kutumia matamshi kutoka kwa Mungu katika mwili kushinda watu wote duniani; Namna hii tu ndiye Mungu katika mwili, na huu tu ndio kuonekana kwa Mungu katika mwili. Labda kwa watu, inaonekana kana kwamba Mungu hajafanya kazi kubwa—lakini Mungu analazimika kutamka maneno Yake ili watu washawishike kabisa, na wao kutishika kabisa. Bila kweli, watu wanapiga makelele na kupiga mayowe; kwa maneno ya Mungu, wote wananyamaza kimya. Mungu hakika atakamilisha ukweli huu, maana huu ni mpango ulioanzishwa na Mungu: kukamilisha ukweli wa Neno kuwasili duniani. Kimsingi, sina haja ya kuelezea—kuwasili kwa Ufalme wa Milenia duniani ni kuwasili kwa neno la Mungu duniani. Kushuka kwa Yerusalemu mpya kutoka mbinguni ni kuwasili kwa maneno ya Mungu kuishi miongoni mwa mwanadamu, kuenenda na kila tendo la mwanadamu, na mawazo yake yote ya ndani. Huu pia ni ukweli kwamba Mungu atatimiza, na mandhari mazuri kabisa ya Ufalme wa Milenia. Huu ndio mpango uliowekwa na Mungu: Maneno Yake yataonekana duniani kwa miaka elfu moja, na yatashuhudia matendo yake yote, na kukamilisha kazi Yake yote duniani, ambapo baada ya hatua hii mwanadamu atakuwa amefikia kikomo.

Uhusiano Wako na Mungu Ukoje?

Katika kumwamini Mungu, angalau lazima utatue suala la kuwa na uhusiano wa kawaida na Mungu. Ikiwa huna uhusiano wa kawaida na Mungu, basi maana ya imani yako katika Mungu imepotea. Kuanzishwa kwa uhusiano wa kawaida na Mungu kunaweza kufikiwa kabisa kwa moyo ulio kimya katika uwepo wa Mungu. Kuwa na uhusiano wa kawaida na Mungu kunamaanisha kuweza kutokuwa na shaka na kutoikana kazi yoyote Yake na kuweza kuitii kazi Yake. Kunamaanisha kuwa na nia zisizo na makosa katika uwepo wa Mungu, kutofanya mipango kwa ajili yako mwenyewe, na kuzingatia masilahi ya familia ya Mungu kwanza katika mambo yote; kunamaanisha kukubali uchunguzi wa Mungu na kuitii mipango ya Mungu. Lazima uweze kuutuliza moyo wako katika uwepo wa Mungu katika yote ufanyayo. Hata kama huyaelewi mapenzi ya Mungu, bado unapaswa kutekeleza wajibu na majukumu yako kadiri uwezavyo. Mara tu mapenzi ya Mungu yanapofichuliwa kwako, lichukulie hatua, na hutakuwa umechelewa mno. Wakati ambapo uhusiano wako na Mungu umekuwa wa kawaida, basi pia utakuwa na uhusiano wa kawaida na watu. Kila kitu kimejengwa kwa msingi wa maneno ya Mungu. Kula na unywe maneno ya Mungu, kisha uyatie matakwa ya Mungu katika vitendo, rekebisha maoni yako, na uepuke kufanya chochote ili kumpinga Mungu au kulivuruga kanisa. Usifanye chochote ambacho hakifaidi maisha ya ndugu zako, usiseme chochote kisichowasidia

wengine, na usifanye jambo lolote la aibu. Kuwa mwenye haki na mwenye heshima katika jambo unalotenda na uhakikishe kuwa kila kitendo chako kinapendeza mbele za Mungu. Ingawa wakati mwingine mwili unaweza kuwa dhaifu, lazima uweze kuweka masilahi ya familia ya Mungu kwanza, bila tamaa ya kupata faida ya kibinafsi, na lazima uweze kutenda kwa haki. Ikiwa unaweza kutenda kwa namna hii, basi uhusiano wako na Mungu utakuwa wa kawaida.

Katika kila jambo unalofanya, sharti uchunguze ikiwa nia zako hazina makosa. Ikiwa unaweza kutenda kulingana na matakwa ya Mungu, basi uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida. Hiki ndicho kiwango cha chini kabisa. Chunguza nia zako, na ukiona kwamba nia mbaya zimejitokeza, uweze kuziacha na kutenda kulingana na maneno ya Mungu; hivyo utakuwa mtu aliye sawa mbele za Mungu, ambayo inaonyesha kwamba uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida, na kwamba yote unayoyafanya ni kwa ajili ya Mungu, si kwa ajili yako. Katika yote unayofanya na yote unayosema, uweze kuuweka moyo wako uwe sawa na uwe mwenye haki katika matendo yako, na usiongozwe na hisia zako, wala kutenda kulingana na mapenzi yako mwenyewe. Hizi ni kanuni ambazowaumini katika Mungu wanapaswa kutenda. Mambo madogo yanaweza kufichua nia na kimo cha mtu, na kwa hivyo, ili mtu aweze kuingia kwenye njia ya kukamilishwa na Mungu, lazima kwanza arekebishe nia zake na uhusiano wake na Mungu. Ni wakati tu uhusiano wako na Mungu unapokuwa wa kawaida ndipo unaweza kukamilishwa na Yeye; ni wakati huo tu ndipo ushughulikiaji, upogoaji, ufundishaji nidhamu, na usafishaji wa Mungu vifanikisha athari zake zilizokusudiwa ndani yako. Hiyo ni kusema, ikiwa wanadamu wanaweza kumweka Mungu mioyoni mwao na wasifuatilie faida ya kibinafsi au kufikiria matarajio yao wenyewe (kwa njia ya mwili), lakini badala yake wabebe mzigo wa kuingia katika uzima, wajitahidi kabisa kuufuatilia ukweli, na kuitii kazi ya Mungu—ikiwa unaweza kufanya hivi, basi malengo unayoyafuatilia yatakuwa sawa, na uhusiano wako na Mungu utakuwa wa kawaida. Kuufanya uhusiano wa mtu na Mungu uwe muwafaka kunaweza kuitwa hatua ya kwanza ya kuingia katika safari ya kiroho ya mtu. Ingawa hatima ya mwanadamu iko mikononi mwa Mungu na imeamuliwa kabla na Mungu, na haiwezi kubadilishwa na mwanadamu, kama unaweza kukamilishwa na Mungu au kupatwa na Yeye kunategemea ikiwa uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida. Kunaweza kuwa na sehemu fulani ndani yako ambazo ni dhaifu au zisizotii—lakini mradi maoni yako na nia zako ni sawa, na mradi uhusiano wako na Mungu uko sawa na wa kawaida, basi unastahili kukamilishwa na Mungu. Ikiwa huna uhusiano muwafaka na Mungu, na unatenda kwa ajili ya mwili au familia yako, basi bila kujali jinsi unavyotia bidii, itakuwa bure. Ikiwa uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida, basi kila kitu kingine kitakuwa sawa. Mungu haangalii kitu kingine chochote, lakini tu ikiwa maoni yako katika imani yako katika Mungu yako sawa: unamwamini nani, unaamini kwa ajili ya nani, na kwa nini unaamini. Ikiwa unaweza kuona mambo haya waziwazi na kutenda

wakati maoni yako yakiwa na mwelekeo mzuri, basi utaendelea katika maisha yako, na pia utahakikishiwa kuingia kwenye njia muwafaka. Ikiwa uhusiano wako na Mungu si wa kawaida, na maoni ya imani yako katika Mungu yamepotoka, basi mengine yote ni bure, na haijalishi kadiri unavyoamini, hutapokea chochote. Ni baada tu ya uhusiano wako na Mungu kuwa wa kawaida ndipo utakapopata sifa kutoka Kwake unapoukana mwili, uombe, uteseke, uvumilie, utii, uwasaidie ndugu zako, ujitumie zaidi kwa ajili ya Mungu, na kadhalika. Kama kile unachofanya kina thamani na umuhimu inategemea ikiwa nia zako ni sawa na maoni yako hazina makosa. Siku hizi, watu wengi wanamwamini Mungu kana kwamba wanageuza vichwa vyao ili kutazama saa—mitazamo yao imepotoka, na lazima irekebishwe kwa mafanikio mapya. Ikiwa shida hii itatatuliwa, kila kitu kitakuwa sawa; la sivyo, kila kitu kitakuwa bure. Watu wengine ni wenye tabia nzuri mbele Zangu, lakini bila Mimi kujua, wananipinga tu. Hili ni onyesho la upotovu na udanganyifu, na mtu wa aina hii ni mtumishi wa Shetani; yeye ni mfano halisi wa Shetani, aliyekuja kumjaribu Mungu. Wewe ni mtu sahihi tu ikiwa unaweza kuitii kazi Yangu na maneno Yangu. Mradi unaweza kula na kunywa maneno ya Mungu; mradi kila kitu unachofanya kinapendeza mbele za Mungu na unaenenda kwa njia ya haki na kwa heshima katika yote unayofanya; mradi hufanyi mambo ya aibu, au mambo ambayo yanaweza kuyadhuru maisha ya wengine; na mradi unaishi katika nuru na hujiruhusu kudhulumiwa na Shetani, basi uhusiano wako na Mungu uko katika mpangilio unaofaa.

Kumwamini Mungu kunakuhitaji uweke nia na maoni yako katika mpangilio unaofaa; unapaswa kuwa na ufahamu muwafaka wa, na njia muwafaka ya kuyachukulia maneno ya Mungu na kazi ya Mungu, mazingira yote ambayo Mungu hupanga, mtu ambaye Mungu humshuhudia, na Mungu wa vitendo. Hupaswi kutenda kulingana na dhana zako mwenyewe au kubuni miradi yako mwenyewe iliyo midogomidogo. Chochote unachofanya, sharti uweze kuutafuta ukweli na, katika nafasi yako kama kiumbe aliyeumbwa, uitii kazi yote ya Mungu. Ikiwa unataka kufuatilia kukamilishwa na Mungu na kuingia kwenye njia muwafaka ya maisha, basi lazima moyo wako uishi katika uwepo wa Mungu daima. Usiwe mwovu, usimfuate Shetani, usimpe Shetani fursa zozote za kutekeleza kazi yake, na usimruhusu Shetani akutumie. Lazima ujitolee kwa Mungu kabisa na umruhusu Mungu akutawale.

Je, uko tayari kuwa mtumishi wa Shetani? Uko tayari kutumiwa vibaya na Shetani?

Unamwamini Mungu na kumfuatilia ili uweze kukamilishwa na Yeye, au ili uweze kuwa foili^[a] kwa ajili ya kazi Mungu? Ungependa maisha yenye kusudi ambayo unapatwa na Mungu, au maisha yasiyofaa na matupu? Ungependa kutumiwa na Mungu, au kudhulumiwa na Shetani?

Ungependa kuruhusu maneno na ukweli wa Mungu vikujaze, au uruhusu kujazwa na dhambi na Shetani? Zingatia mambo haya kwa uangalifu. Katika maisha yako ya kila siku, lazima uelewe ni maneno gani unayoyasema na ni mambo gani unayoyafanya ndiyo yanaweza kusababisha

hitilafu katika uhusiano wako na Mungu, na kisha ujibadilishe ili uingie katika njia muwafaka. Wakati wote, yachunguze maneno yako, matendo yako, kila harakati yako, na mawazo na maoni yako yote. Pata ufahamu muwafaka kuhusu hali yako halisi na uingie katika njia ya kazi ya Roho Mtakatifu. Hii ndiyo njia ya pekee ya kuwa na uhusiano wa kawaida na Mungu. Kwa kutathmini kama uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida, utaweza kurekebisha nia zako, kuelewa asili na kiini cha mwanadamu, na kujielewa kwa kweli, na kwa kufanya hivyo, utaweza kuingia katika matukio halisi, ujikane kwa njia halisi, na kutii kwa kusudi. Unapopitia mambo haya kuhusu ikiwa uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida au la, utapata fursa za kukamilishwa na Mungu na kuweza kufahamu hali nyingi za kazi ya Roho Mtakatifu. Pia utaweza kubaini hila nyingi za Shetani na kufahamu njama zake. Njia hii tu ndiyo inayosababisha kukamilishwa na Mungu. Rekebisha uhusiano wako na Mungu, ili uweze kutii mpangilio Wake kwa ukamilifu, na ili uweze kuingia kwa undani hata zaidi katika matukio halisi na kupokea kazi zaidi ya Roho Mtakatifu. Ukijizoeza kuwa na uhusiano wa kawaida na Mungu, mara nyingi, mafanikio yatapatikana kwa kuukana mwili na kupitia kwa ushirikiano wa kweli na Mungu. Unapaswa kuelewa kwamba “bila moyo wa kushirikiana, ni vigumu kuipokea kazi ya Mungu; ikiwa mwili hautateseka, hakutakuwa na baraka kutoka kwa Mungu; ikiwa roho haijitahidi sana, Shetani hataaibishwa.” Ukifuata kanuni hizi na uzielewe kabisa, maoni ya imani yako katika Mungu yatarekebishwa. Katika kutenda kwako kwa sasa, lazima uache fikira ya “kutafuta mkate ili kukidhi njaa”; lazima uache fikira ya “kila kitu kinafanywa na Roho Mtakatifu, na watu hawawezi kuingilia kati.” Kila mtu asemaye hivyo hufikiria, “Watu wanaweza kufanya chochote watakacho, na wakati ufikapo, Roho Mtakatifu atafanya kazi Yake. Watu hawana haja ya kuuzuia mwili au kushirikiana; jambo la maana ni kwamba waguswe na Roho Mtakatifu.” Maoni haya yote ni ya kipumbavu. Katika hali kama hizo, Roho Mtakatifu hawezi kufanya kazi. Ni mtazamo wa aina hii ndio unaoizuia sana kazi ya Roho Mtakatifu. Mara nyingi, kazi ya Roho Mtakatifu hufikiwa kupitia ushirikiano wa binadamu. Wale ambao hawashirikiani na hawajaamua, ilhali wanataka kupata mabadiliko katika tabia yao na kuipokea kazi ya Roho Mtakatifu na nuru na mwangaza kutoka kwa Mungu, wana mawazo ya kupita kiasi kweli. Hii inaitwa “kujifurahisha na kumsamehe Shetani.” Watu kama hao hawana uhusiano wa kawaida na Mungu. Unapaswa kuona ufunuo na udhihirisho mwingi wa tabia ya kishetani ndani yako mwenyewe na uone mazoea yoyote ambayo unayo yaliyo kinyume na kile ambacho Mungu anahitaji sasa. Je, sasa utaweza kumkana Shetani? Unapaswa kufikia uhusiano wa kawaida na Mungu, kutenda kulingana na nia ya Mungu, na kuwa mtu mpya aliye na maisha mpya. Usifikiri sana kuhusu makosa ya zamani; usiwe mwenye kujuta mno; uweze kusimama na kushirikiana na Mungu, na utimize wajibu unaopaswa kutimiza. Kwa njia hii, uhusiano wako na Mungu utakuwa wa kawaida.

Ikiwa baada ya kusoma makala haya, unadai tu kukubali maneno haya, ilhali moyo wako hauguswi, na hutafuti kufanya uhusiano wako na Mungu uwe wa kawaida, inathibitisha kwamba hutilii maanani uhusiano wako na Mungu. Inathibitisha kwamba maoni yako bado hayajarekebishwa, kwamba nia zako bado hazijadhamiria kupatwa na Mungu na kumletea Yeye utukufu, lakini badala yake zimedhamiria kuruhusu njama za Shetani zitawale na kufanikisha malengo yako mwenyewe. Watu kama hao wanahodhi nia mbaya na maoni yaliyo na makosa. Haijalishi lile analosema Mungu au jinsi Anavyolisema, watu kama hao hubaki wasiojali kabisa na hawabadiliki hata kidogo. Mioyo yao haihisi woga na wao hawaoni haya. Mtu kama huyo ni mjinga aliyekata tamaa. Soma matamko yote ya Mungu na uyatie katika vitendo mara tu utakapoyaelewa. Labda kulikuwa na nyakati ambapo mwili wako ulikuwa dhaifu, au ulikuwa mwasi, au ulipinga; bila kujali jinsi ulivyotenda zamani, si muhimu, na haiwezi kuyazuia maisha yako kukomaa leo. Mradi unao uhusiano wa kawaida na Mungu leo, kuna matumaini. Ikiwa kuna mabadiliko ndani yako kila wakati unapoyasoma maneno ya Mungu, na wengine wanaweza kukuambia kuwa maisha yako yamebadilika na kuwa bora, inaonyesha kuwa uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida sasa, kwamba umerekebishwa. Mungu hawatendei watu kulingana na makosa yao. Mara tu unapoelewa na kufahamu, mradi unaweza kuacha kuasi au kupinga, basi bado Mungu atakuonea huruma. Unapokuwa na ufahamu na azimio la kufuatilia kukamilishwa na Mungu, basi hali yako katika uwepo wa Mungu itakuwa ya kawaida. Haijalishi unachofanya, fikiria yafuatayo wakati unapofanya jambo hilo: Je, Mungu atafikiria nini nikifanya hili? Litawafaidi ndugu zangu? Litaifaidi kazi katika nyumba ya Mungu? Iwe ni katika sala, ushirika, hotuba, kazi, au kuwasiliana na wengine, zichunguze nia zako, na uchunguze ikiwa uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida. Ikiwa huwezi kutambua nia na mawazo yako mwenyewe, hii inamaanisha kuwa huna upambanuzi, ambayo inathibitisha kwamba unaelewa ukweli kidogo sana. Ikiwa unaweza kuelewa vizuri kila kitu ambacho Mungu hufanya, na unaweza kuyatazama mambo kupitia katika maneno Yake, ukisimama upande Wake, basi maoni yako yatakuwa yamekuwa yasiyo na makosa. Kwa hivyo, kuanzisha uhusiano mzuri na Mungu ni muhimu sana kwa mtu yeyote anayemwamini Mungu; kila mtu anapaswa kuliona kama kazi muhimu sana na tukio kubwa kabisa katika maisha yake. Kila kitu unachofanya kinapimwa na kama una uhusiano wa kawaida na Mungu. Ikiwa uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida na nia zako ni zisizo na makosa, basi chukua hatua. Ili kudumisha uhusiano wa kawaida na Mungu, hupaswi kuogopa kupata hasara kwa masilahi yako ya kibinafsi; huwezi kumruhusu Shetani atawale, huwezi kumruhusu Shetani akununue, na huwezi kumruhusu Shetani akufanye uwe kichekesho. Kuwa na nia kama hiyo ni ishara kwamba uhusiano wako na Mungu ni wa kawaida—si kwa ajili ya mwili, bali ni kwa ajili ya amani ya roho, kwa ajili ya kuipata kazi ya Roho Mtakatifu, na kwa ajili ya kuyaridhisha mapenzi ya Mungu. Ili kuingia katika hali inayofaa, lazima uimarisha uhusiano mzuri na Mungu na urekebishe maoni ya imani yako katika

Mungu. Hii ni ili Mungu aweze kukupata, na ili Aweze kudhihirisha matunda ya maneno Yake ndani yako na kukupa nuru na kukuangazia hata zaidi. Kwa njia hii, utakuwa umeingia katika njia inayofaa. Endelea kula na kunywa maneno ya Mungu ya leo, ingia katika njia ya sasa ya Roho Mtakatifu ya kufanya kazi, tenda kulingana na matakwa ya Mungu ya leo, usifuate mbinu za zamani za kutenda, usishikilie njia za zamani za kufanya mambo, na uingie katika njia ya leo ya kufanya kazi haraka iwezekanavyo. Hivyo, uhusiano wako na Mungu utakuwa wa kawaida kabisa na utakuwa umeanza kutembea katika njia muwafaka ya imani katika Mungu.

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha

Sisitiza Uhalisi Zaidi

Kila mtu ana uwezekano wa kukamilishwa na Mungu, kwa hiyo kila mtu anapaswa kuelewa ni huduma gani kwa Mungu ndiyo inayolingana zaidi na makusudi Yake. Watu wengi hawajui kumwamini Mungu humaanisha nini na hawajui kwa nini wanapaswa kumwamini Yeye—yaani, wengi zaidi hawana ufahamu wa kazi ya Mungu au lengo la mpango Wake wa usimamizi. Leo, watu wengi zaidi bado wanadhani kumwamini Mungu kunahusu kwenda mbinguni na roho zao kuokolewa. Bado hawajui chochote kuhusu umuhimu mahususi wa kumwamini Mungu, na aidha hawana ufahamu wowote wa kazi muhimu kabisa ya Mungu katika mpango Wake wa usimamizi. Kwa sababu zao mbali mbali za kibinafsi, watu hawavutiwi kabisa na kazi ya Mungu wala hawatafakari juu ya makusudi ya Mungu au mpango wa Mungu wa usimamizi. Kama mtu binafsi katika mkondo huu, kila mtu anapaswa kujua lengo la mpango mzima wa usimamizi wa Mungu ni nini, ukweli ambao Mungu tayari ametimiza, kwa nini Amelichagua kundi hili la watu, malengo na umuhimu wa Yeye kuwachagua ni upi, na kile ambacho Anataka kufanikisha katika kundi hili. Mungu kuweza kuliinua kundi kama hilo la watu wasiofika katika nchi ya joka kubwa jekundu na kuweza kuendelea kufanya kazi hadi sasa, Akijaribu na kuwakamilisha kwa kila namna, Akizungumza maneno yasiyohesabika, Akitekeleza kazi kubwa na kutuma vitu vingi vya kuhudumu—kwa Mungu pekee kuweza kukamilisha kazi kubwa kama hiyo inaonyesha jinsi kazi Yake ilivyo muhimu. Kwa sasa, huna uwezo wa kuelewa hili kikamilifu. Hivyo, ni sharti msiichukulie kazi ambayo Mungu amefanya ndani yenu kama jambo dogo; hili si jambo dogo. Hata kile ambacho Mungu amewafichulia leo kinawatosha kujaribu kutafakari na kujua. Mkielewa tu kwa kweli na kwa kina ndipo matukio yenu yatakuwa ya kina na maisha yenu yatakua. Leo, watu wanaelewa na kufanya kidogo sana; hawana uwezo wa kutimiza makusudi ya Mungu kikamilifu. Huu ni upungufu wa wanadamu na kushindwa kwao kutimiza wajibu wao, hivyo, hawawezi kutimiza matokeo yanayotarajiwa. Roho Mtakatifu hana njia ya kufanya kazi ndani ya watu wengi kwa sababu wana ufahamu wa juu juu wa kazi ya Mungu na hawako tayari

kuichukulia kazi ya nyumba ya Mungu kama kitu fulani cha thamani wanapoifanya. Siku zote wanafanya vitu kwa namna isiyo ya dhiti ili wapate kuishi tu, au vinginevyo kuiga kile ambacho watu wengi zaidi wanafanya, au kufanya kazi tu kwa ajili ya maonyesho. Leo, kila mtu katika mkondo huu anapaswa kukumbuka iwapo katika matendo na vitendo vyake, kile ambacho amefanya kila ambacho angeweza kufanya, na iwapo ametia bidii zake zote. Watu wameshindwa kabisa kutimiza wajibu wao, si kwa sababu Roho Mtakatifu hafanyi kazi Yake bali kwa sababu watu hawafanyi kazi yao, wakifanya isiwezekane kwa Roho Mtakatifu kufanya kazi Yake. Mungu hana maneno zaidi ya kunena, lakini watu hawajaenda kwa kasi sawa kabisa, na wamebaki nyuma kabisa, hawawezi kukaa karibu na kila hatua, hawawezi kuzifuata nyayo za Mwanakondoo kwa karibu. Kile ambacho walipaswa kukitii hawajakitii; kile ambacho walipaswa kukitenda hawajakitenda; kile ambacho walipaswa kukiomba hawajakiomba; kile ambacho walipaswa kukiacha hawajakiacha. Bado hawajafanya kitu chochote kati ya hivi. Kwa hiyo, mazungumzo haya ya kuhudhuria karamu ni maneno matupu; hayana maana yoyote halisi na yote yamo katika fikira zao. Ikitazamwa kutoka leo, inaweza kusemwa kwamba hadi sasa watu hawajitimiza wajibu wao hata kidogo. Kila kitu kinategemea Mungu kufanya na kusema vitu Yeye Mwenyewe. Kazi ya mwanadamu kwa kweli imekuwa ndogo sana; watu ni taka isiyokuwa na maana ambao hawana uwezo wa kushirikiana na Mungu. Mungu amenena mamia ya maelfu ya maneno, lakini watu hawajayaweka katika vitendo kabisa—iwe ni kuukana mwili, kuacha dhana, kuwa watiifu kwa Mungu katika mambo yote huku ukikukuza ufahamu na kupata umaizi, kutowapa watu nafasi mioyoni mwao, kuondoa sanamu ambazo zinamiliki mioyo yao, kuasi dhidi ya makusudi yao binafsi ambayo si sahihi, kutotenda kwa msingi wa mihemko yao, kufanya mambo kwa haki na bila ubaguzi, kuyafikiria zaidi masilahi ya Mungu na ushawishi wao kwa wengine wanapozungumza, kufanya mambo zaidi yanayonufaisha kazi ya Mungu, kufikiri kuhusu kuinufaisha nyumba ya Mungu katika yote wanayofanya, kutoruhusu mihemko yao ziamuru tabia yao, kuacha yale ambayo yanapendeza miili yao wenyewe, kuondoa maoni ya zamani ya ubinafsi, na kadhalika. Kwa kweli watu wanafahamu baadhi ya mahitaji haya ambayo Mungu anahitaji kutoka kwa mwanadamu, lakini hawako tayari kuyaweka katika vitendo. Ni kwa namna gani nyingine ambayo Mungu anaweza kufanya kazi na kuwashawishi? Waasi machoni pa Mungu wanawezaje bado kuwa na ujasiri wa kuchukua maneno Yake na kuyastahi? Wanawezaje kuwa na ujasiri wa kula chakula cha Mungu? Dhamiri ya watu ipo wapi? Hawajitimiza wajibu mdogo kabisa waliopaswa kutimiza, sembuse kufanya yote wawezayo. Je, wao si watu wa njozi tu? Hakuwezi kuwa na mazungumzo ya uhalisi bila matendo. Huo ni ukweli wa wazi!

Mnapaswa kuwa mkijifunza mafunzo yaliyo ya uhalisi zaidi. Hakuna haja ya hayo mazungumzo matupu, yenye kuvutia na ambayo watu wanayastahi. Linapokuja suala la kuzungumza kuhusu

maarifa, ya kila mtu ni ya juu kuliko ya aliyetangulia, lakini bado hawana njia ya kutenda. Ni watu wangapi wameelewa kanuni za kutenda? Ni wangapi wamejifunza mafunzo halisi? Ni nani anayeweza kufanya ushirika kuhusu uhalisi? Kuweza kuzungumza juu ya maarifa ya maneno ya Mungu si sawa na kimo chako halisi. Hilo linaishia kuonyesha tu kuwa ulizaliwa ukiwa na akili, kwamba wewe una kipaji. Ikiwa huwezi kuonyesha njia, basi matokeo yatakuwa bure, na wewe utakuwa taka isiyo na maana! Je, hujifanyi tu ikiwa huwezi kusema chochote kuhusu njia halisi ya kufanya vitendo? Je, hujifanyi ikiwa huwezi kutoa uzoefu wako mwenyewe halisi kwa wengine, na hivyo kuwapa mafunzo ambayo wanaweza kujifunza kwayo au njia ya kufanya vitendo? Je, wewe si bandia tu? Una thamani gani? Mtu kama huyo angeweza tu kushikilia sehemu ya kuwa “mvumbuzi wa nadharia ya ujamaa,” na si “mchangiaji wa kuleta ujamaa.” Kutokuwa na uhalisi ni kutokuwa na ukweli. Kutokuwa na uhalisi ni kutokuwa na thamani. Kutokuwa na uhalisi ni kukosa uhai. Kutokuwa na uhalisi ni “kuwa na fikira za Umaksi na Ulenini,” bila thamani kama marejeo. Ninamsihi kila mtu kufunga mdomo kuhusu nadharia na kuzungumzia kitu ambacho ni halisi, kitu ambacho ni cha kweli na thabiti, kujifunza baadhi ya “sanaa za kisasa,” kusema kitu ambacho ni halisi, kuchangia uhalisi kiasi, na kuwa na roho ya kujitoa. Uukabili uhalisi unapozungumza; usijiingize katika mazungumzo yasiyokuwa na uhalisi na yaliyotiwa chumvi ili kuwafurahisha watu au wakae na kukustahi. Thamani yake ni nini? Kuna maana gani katika kuwafanya watu kukutendea kwa ukunjufu? Kuwa “stadi” kiasi katika usemi wako, tenda haki zaidi kiasi katika matendo yako, kuwa mwenye busara zaidi kiasi katika jinsi unavyoshughulikia vitu, kuwa mwenye vitendo zaidi kiasi katika kile unachosema, fikiri kuhusu kuleta manufaa kwa nyumba ya Mungu katika kila tendo, acha dhamiri yako unapokuwa na muhemuko, usilipize wema kwa chuki, au kutokuwa na shukrani kwa wema, na usiwe mnaifiki, usije ukawa na “ushawishi mbaya.” Unapokula na kunywa maneno ya Mungu, yahusishe zaidi na uhalisi, na unapowasiliana, zungumza zaidi kuhusu mambo ya uhalisi. Usijikweze; Mungu hataridhishwa na hilo. Katika miingiliano yako na wengine, kuwa mstahimilivu zaidi, fanya mazoezi zaidi ya kukubali, kuwa mkarimu zaidi kiasi, na ujifunze kutoka kwa “roho ya waziri mkuu.”^[a] Unapokuwa na mawazo ambayo si mazuri, fanya mazoezi zaidi ya kuukana mwili zaidi. Unapofanya kazi, zungumza zaidi kuhusu njia halisi na usiwe na majivuno sana, vinginevyo kile unachosema hakitaweza kufikiwa na watu. Starehe kidogo, mchango zaidi—onyesha roho yako ya kujitolea isiyo ya ubinafsi. Fikirieni zaidi makusudi ya Mungu, sikilizeni dhamiri zenu zaidi, kuweni wenye kuzingatia zaidi, na msisahau jinsi ambavyo Mungu huwanenea kila siku kwa uvumilivu na kwa dhati. Soma “shajara ya mwaka ya zamani” mara kwa mara. Omba zaidi na ufanye ushirika mara kwa mara. Usiendeleo kuwa mtu aliyekanganyikiwa sana, bali onyesha busara zaidi na upate umaizi fulani. Mkono wa dhambi unaponyooka, urudishe nyuma na usiuache utandae zaidi. Haina maana! Mnachokipata kutoka kwa Mungu si chochote bali laana; kuweni waangalifu. Acheni mioyo yenu iwe na huruma kwa

wengine na siku zote msiwapige kwa silaha mkononi. Shirikini zaidi kuhusu maarifa ya ukweli na mzungumze zaidi kuhusu maisha, mkiwa na roho ya kuwasaidia wengine. Tendeni zaidi na kusema kidogo. Tieni mengi zaidi katika vitendo na kidogo katika utafiti na uchambuzi. Acheni mguswe zaidi na Roho Mtakatifu, na mpeni Mungu fursa zaidi ya kuwakamilisha. Ondoeni sifa zaidi za kibinadamu; bado mna sifa nyingi za kibinadamu za kufanya mambo na matendo na namna yenu ya juujuu ya kufanya bado ni ya kuwachukiza wengine: Ziondoeni hizi zaidi. Hali zenu za akili bado zinachukiza sana; tumieni muda zaidi kuzirekebisha. Bado mnawapa watu hadhi kuu; mpeni Mungu hadhi zaidi, na usiwe mtu usiyekuwa na akili. “Hekalu” limekuwa la Mungu daima na halipaswi kutwaliwa na watu. Kwa ufupi, sisitiza zaidi juu ya haki na kidogo katika mihemuko. Ni bora zaidi kuuondoa mwili. Zungumza zaidi kuhusu uhalisi na kidogo kuhusu maarifa; kilicho bora zaidi kuwa kimya na kutosema lolote. Zungumza zaidi juu ya njia ya kutenda na ufanyemajivuno kidogo zaidi yasiyo na thamani. Itakuwa bora zaidi kuanza kutenda sasa.

Matakwa ya Mungu kwa watu si ya juu sana. Ikiwa watu wataweka hata jitihada kidogo wataweza kupata “alama ya kupita.” Kwa kweli, kufahamu, kujua, na kuelewa ukweli kunatatiza sana kuliko kuutenda ukweli; kuujua na kuutambua ukweli kunakuja baada ya kuutenda ukweli; hizi ndizo hatua na njia ambayo kwayo Roho Mtakatifu hufanya kazi. Unawezaje kutotii? Je, unaweza kupata kazi ya Roho Mtakatifu kwa kufanya mambo kwa namna yako? Je, Roho Mtakatifu hufanya kazi kwa kuzingatia ridhaa yako, au kwa msingi wa kasoro zako kulingana na maneno ya Mungu? Haina maana ikiwa huwezi kuliona hili kwa uwazi. Kwa nini watu wengi zaidi wametumia jitihada nyingi kusoma maneno ya Mungu lakini wana maarifa tu na hawawezi kusema kitu chochote kuhusu njia halisi baada ya hapo? Unadhani kwamba kuwa na maarifa ni sawa na kuwa na ukweli? Je, huo si mtazamo uliokanganywa? Unaweza kuzungumza maarifa mengi kama mchanga ulivyo ufuoni, lakini hakuna yaliyo na njia ya kweli. Je, wewe hujaribu kuwapumbaza watu kwa kufanya hivi? Je, unafanya maonyesho matupu, bila dutu ya kuyasitiri? Mienendo yote kama hii ni ya madhara kwa watu! Kadiri nadharia inavyokuwa ya juu, ndivyo inavyokosa uhalisi zaidi, na ndivyo inavyokosa zaidi uwezo wa kuwapeleka watu katika uhalisi; kadiri nadharia inavyokuwa ya juu, ndivyo inavyokufanya umuasi na kumpinga Mungu. Usizichukulie nadharia za kiwango cha juu kama hazina ya thamani; zina madhara, na hazina kazi yoyote! Pengine baadhi ya watu wanaweza kuzungumza juu ya nadharia za juu sana—lakini nadharia hizo hazina kitu chochote cha uhalisi, maana watu hawajazipitia wao binafsi, na kwa hiyo hawana njia ya kutenda. Watu kama hao hawawezi kuwaongoza wengine katika njia sahihi, na watawapotosha. Je, hili halileti madhara kwa watu? Angalau kabisa, unapaswa kuweza kutatua shida za sasa za watu na kuwaruhusu kupata kuingia; hii tu ndiyo inachukuliwa kama ibada, na baada ya hapo ndipo utakuwa na sifa za kufaa kumfanyia Mungu kazi. Siku zote

usizungumze maneno ya kifahari, ya ajabu, na usiwalazimishe watu kukutii wewe pamoja na vitendo vyako visivyofaa. Kufanya hivyo hakutaleta matokeo, na kunaweza kuongeza tu mkanganyiko wa watu. Kuendelea kwa namna hii kutazalisha mafundisho mengi, ambazo zitawafanya watu wakuchukie. Hivyo ndivyo ulivyo udhaifu wa mwanadamu, na kwa kweli unadhalilisha. Kwa hivyo, zungumza zaidi juu ya matatizo ambayo yapo kwa kweli. Usiyachukulie matukio ya watu wengine kama mali yako binafsi na kuyaonyesha waziwazi ili wengine wastahi; unapaswa kutafuta suluhisho lako binafsi mwenyewe. Hiki ndicho ambacho kila mtu anapaswa kuweka katika vitendo.

Ikiwa kile unachoshiriki kinaweza kuwapa watu njia ya kufuata, basi hiyo ni sawa na wewe kuwa na uhalisi. Haijalishi kile unachosema, ni lazima uwaletе watu katika vitendo na kuwapatia njia wanayoweza kuifuata. Usiwaruhu tu wapate maarifa; lililo muhimu zaidi ni kuwa na njia ya kufuata. Ili watu wamwamini Mungu, lazima waitembe njia inayoongozwa na Mungu katika kazi Yake. Yaani, mchakato wa kumwamini Mungu ni mchakato wa kuitembea njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu. Vivyo hivyo, unapaswa kuwa na njia ambayo unaweza kuitembea kwa vyovyote vile, na unapaswa kuenenda kwenye njia ya kukamilishwa na Mungu. Usibaki nyuma sana, na usijishughulishe na mambo mengi sana. Ikiwa tu unaitembea njia inayoongozwa na Mungu bila kusababisha mwingiliano ndipo unaweza kupokea kazi ya Roho Mtakatifu na kuwa na njia ya kuingia. Hili tu ndilo linahesabika kama lenye kufaa makusudi ya Mungu na kutimiza wajibu wa binadamu. Kama mtu binafsi katika mkondo huu, kila mtu anapaswa kutimiza wajibu wake kikamilifu, fanya zaidi yale ambayo watu wanapaswa kuyafanya, na usitende kwa ukaidi. Watu wanaotekeleza kazi wanapaswa kuweka maneno yao wazi, watu wanaofuata wanapaswa kusesitiza zaidi kuhimili ugumu na kutii, na kila mtu anapaswa kutunza nafasi yake na kutotenda kwa namna isiyofaa. Linapaswa lieleweke wazi katika moyo wa kila mtu namna ambavyo wanapaswa kutenda na ni kazi gani wanapaswa kutimiza. Chukua njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu; usipotoke au kukosea. Lazima muione kazi ya leo waziwazi. Kuingia katika njia ya leo ya kufanya kazi ndicho kitu mnachopaswa kutenda. Ni kitu cha kwanza mnachopaswa kuingia. Msipoteze maneno yoyote zaidi kwenye mambo mengine. Kufanya kazi ya nyumba ya Mungu leo ni jukumu lenu, kuingia katika mbinu ya kazi ya leo ni wajibu wenu, na kutenda ukweli wa leo ni mzigo wenu.

Tanbihi:

a. Roho ya waziri mkuu: Ni msemo wa jadi wa Kichina ambao hutumika kuelezea mtu ambaye ni mkarimu na anayekubali mawazo ya wengine.

Kuzishika Amri na Kuutenda Ukweli

Katika matendo, kushika amri zapaswa kuunganishwa na matendo ya ukweli. Wakati

unapozishika amri, mtu anapaswa kutenda ukweli. Wakati anapotenda ukweli, mtu hapaswi kukiuka kanuni za amri au kwenda kinyume na amri. Fanya yale ambayo Mungu anahitaji uyafanye. Kuzishika amri na kuutenda ukweli vinahusiana, bali havikinzani. Zaidi unavyotenda ukweli, ndivyo unavyoweza kutilia maanani zaidi kiini cha amri. Zaidi unavyotenda ukweli, ndivyo utakavyoweza kulielewa zaidi neno la Mungu kama ilivyoonyeshwa katika amri. Kutenda ukweli na kuzishika amri sio vitendo vinavyopingana, lakini badala yake vinahusiana. Mwanzoni, ni kwa kuzishika tu amri ndipo mwanadamu anaweza kuutenda ukweli na kufikia kuipata nuru kutoka kwa Roho Mtakatifu. Lakini hii sio nia ya awali ya Mungu. Mungu inakuhitaji umwabudu Mungu kwa moyo, sio tu kutenda tabia nzuri. Lakini lazima uzishike amri angalau hivi hivi. Hatua kwa hatua, kupitia uzoefu, mwanadamu hupata ufahamu wa wazi zaidi wa Mungu. Yeye huacha kumwasi na kumpinga Mungu, naye anaacha kuitilia shaka kazi ya Mungu. Kwa njia hii mtu anaweza kuzingatia kiini cha amri. Kwa hiyo, kuzishika tu amri bila kutenda ukweli ni hafifu nako hakufanyizi ibada ya kweli ya Mungu kwa sababu bado hujafikia kimo cha kweli. Ukizishika amri bila ukweli, hii ni sawa na kuzingatia tu sheria bila kushawishika. Katika kufanya hivyo, amri zinakuwa sheria yako, ambayo haitakusaidia kukua katika maisha. Badala yake, zitakuwa mzigo wako, nazo zitakufunga imara kama sheria ya Agano la Kale, zikusababishe kuupoteza uwepo wa Roho Mtakatifu. Kwa hiyo, ni kwa kuutenda ukweli tu ndipo utakapoweza kuzishika amri kwa ufanisi. Mtu huzishika amri ili autende ukweli. Unautenda hata ukweli zaidi kwa kuzishika amri. Unapata hata uelewa zaidi wa maana halisi ya amri kwa kuutenda ukweli. Kusudi na maana ya sharti la Mungu ni kwamba lazima mwanadamu azishike amri sio kuzifuata sheria kama mwanadamu anavyoweza kufikiria, lakini inahusiana na mwanadamu kuingia katika maisha. Zaidi unavyokua katika maisha, ndivyo unapata kiwango kibukwa zaidi ambacho utaweza kutii amri. Ingawa amri ni za mwanadamu kuzishika, asili ya amri inakuwa tu dhahiri kupitia kwa uzoefu wa maisha ya mwanadamu. Watu wengi wanadhani kwamba kuzishika amri vizuri inamaanisha “kila kitu kiko tayari, kile kimebaki ni kuchukuliwa juu.” Huku ni kufikiria badhirifu nako sio mapenzi ya Mungu. Wale wanaosema mambo kama haya hawataki kufanya maendeleo nao wanayo tamaa ya mwili. Hili halina maana! Hili haliambatani na uhalisi! Siyo mapenzi ya Mungu kutenda ukweli tu bila kushika amri kwa kweli. Wale wanaofanya hivi ni vilema; wao ni kama watu wasio na mguu mmoja. Wakifuata tu amri kana kwamba wanafuata masharti, lakini hawana ukweli—huku si kuridhisha mapenzi ya Mungu, pia; kama kama wale wasio na jicho moja, watu wanaofanya hivi pia, wanateseka kwa ajili ya aina fulani ya ulemavu. Inaweza kusemwa kwamba ukizishika amri vizuri na kupata uelewa wa wazi wa Mungu wa vitendo, basi utakuwa na ukweli. Kutokana na mtazamo wa uhusiano, utakuwa umepata kimo cha kweli. Unatenda ukweli unaopaswa kutenda na kuzishika amri kwa wakati mmoja bila migogoro ya pande zote. Kuutenda ukweli na kuzishika amri ni mifumo miwili, yote ambayo ni sehemu muhimu ya uzoefu wa maisha ya mtu. Uzoefu wa mtu

lazima uafikiane na muungano wa kuzishika amri kwa kuutenda ukweli, sio kugawanya. Hata hivyo, kunazo tofauti na uhusiano kati ya mambo haya mawili.

Kutangazwa rasmi kwa amri katika enzi mpya ni ushahidi wa ukweli kwamba wanadamu wote katika mkondo huu na wale ambao husikia sauti ya Mungu leo wameingia katika enzi mpya. Huu ni mwanzo mpya kwa ajili ya kazi ya Mungu nao ni mwanzo wa sehemu ya mwisho ya kazi katika mpango wa usimamizi wa Mungu katika kipindi cha miaka elfu sita. Amri za enzi mpya zinaashiria kuwa Mungu na binadamu wameingia katika eneo la mbingu mpya na nchi mpya, na kwamba Mungu, kama vile Yehova alifanya kazi miongoni mwa Waisraeli naye Yesu alifanya kazi miongoni mwa Wayahudi, Ataifanya kazi zaidi ya vitendo na kuifanya kazi zaidi na kubwa zaidi duniani. Pia zinaashiria kwamba kundi hili la watu watapokea agizo zaidi na kubwa zaidi kutoka kwa Mungu, nao watapokea ugavi wa vitendo, malisho, msaada, huduma na ulinzi kutoka kwa Mungu. Zaidi ya hayo watafanywa kupitia katika mazoezi zaidi ya vitendo, na pia kushughulikiwa, kuvunjwa na kusafishwa kwa neno la Mungu. Maana ya amri za enzi mpya ni kubwa sana. Zinaonyesha kwamba Mungu kweli ataonekana kwenye ardhi naye Mungu ataushinda ulimwengu mzima juu ya nchi, akiuonyesha utukufu Wake wote katika mwili. Pia zinaonyesha kwamba Mungu wa vitendo anaenda kuifanya kazi zaidi ya vitendo duniani ili akamilishe yote ambayo Amechagua. Zaidi ya hayo, Mungu atatimiza kila kitu kwa maneno duniani na kufanya wazi amri kwamba “Mungu mwenye mwili huinuka juu zaidi naye ametukuzwa, nao watu wote na mataifa yote hupiga magoti kumwabudu Mungu—ambaye ni mkuu.” Ingawa amri za enzi mpya ni za mwanadamu kuzishika, na ingawa kufanya hivyo ni wajibu wa mwanadamu na jukumu lake, maana ambazo zinawakilisha ni ya kina sana kuweza kuonyeshwa kikamilifu katika neno moja au mawili. Amri za enzi mpya zinachukua nafasi ya sheria za Agano la Kale na maagizo ya Agano Jipya kama zilivyotangazwa rasmi na Yehova na Yesu. Hili ni somo la ndani zaidi, sio jambo rahisi kama mtu anavyoweza kufikiria. Amri za enzi mpya zinazo kipengele cha maana ya vitendo: Zinatumika kama kipengee kinachojitokeza kati ya Enzi ya Neema na Enzi ya Ufalme. Amri za enzi mpya zinahitimisha mazoea yote na maagizo yote ya enzi ya zamani na pia zinahitimisha mazoea yote ya enzi ya Yesu na zile kabla yake. Zinamleta mwanadamu katika uwepo wa Mungu wa vitendo zaidi na kumruhusu mtu kuanza kuupokea ukamilifu wa binafsi wa Mungu, ambazo ni mwanzo wa njia ya kukamilika. Kwa hiyo, ninyi mtamiliki mtazamo sahihi kuelekea amri za enzi mpya na wala hamtazuifuta ovyo wala kuzidharau. Amri za enzi mpya zinasisitiza hoja moja: kwamba mwanadamu atamwabudu Mungu wa vitendo Mwenyewe wa leo, ambayo ni kutii kiini cha Roho katika matendo zaidi. Pia zinasisitiza kanuni ambayo Mungu atamhukumu mwanadamu kuwa na hatia au haki Atakapoonekana kama Jua la haki. Amri zinaeleweka kwa urahisi kuliko kutendwa. Hivyo, kama Mungu anataka kumkamilisha mwanadamu, lazima Atafanya hivyo kupitia kwa maneno Yake

mwenyewe na mwongozo, mwanadamu hawezi kufikia ukamilifu kupitia asili ya akili yake peke yake. Ikiwa mwanadamu anaweza kuzishika amri za enzi mpya au la inahusiana na maarifa ya mwanadamu ya Mungu wa vitendo. Kwa hiyo, kama unaweza kuzishika amri au la sio swali litakalotatuliwa katika siku chache. Hili ni somo la kina.

Kuutenda ukweli ni njia ambayo kwayo maisha ya mwanadamu yanaweza kukua. Msipotenda ukweli, mtaachwa na nadharia tu nanyi hamtakuwa na maisha ya kweli. Ukweli ni ishara ya kimo cha mwanadamu. Ikiwa hauutendi ukweli au la inahusiana na kufikia kimo cha kweli. Kama hauutendi ukweli, hutendi kwa haki, au unashawishiwa na hisia na kuujali mwili, basi uko mbali na kuzishika amri. Hili ni somo la kina zaidi. Kunazo kweli nyingi kwa mwanadamu kuingia na mwanadamu kuelewa katika kila enzi. Lakini kunazo amri mbalimbali zinazoambatana na ukweli katika kila enzi. Ukweli ambao mwanadamu huutenda unahusiana na enzi na amri zinazowekwa na mwanadamu pia huhusiana na enzi. Kila enzi inazo kweli zake ambazo lazima zitendwe na amri za kuhifadhiwa. Hata hivyo, kulingana na amri mbalimbali ambazo zimetangazwa rasmi na Mungu, ambayo ni, kulingana na enzi tofauti, lengo na athari ya kuutenda ukweli kwa mwanadamu vinatofautiana kwa kadri iliyo sawa. Inaweza kusemwa kwamba amri huutumikisha ukweli nao ukweli huwepo kuzidumisha amri. Kama kuna ukweli tu, hakutakuwa na mabadiliko katika kazi ya Mungu kuyataja. Hata hivyo, kwa kuzirejelea amri, mwanadamu anaweza kutambua ukubwa wenye nguvu wa kazi iliyofanywa na Roho Mtakatifu naye mwanadamu anaweza kujua enzi ambayo Mungu hufanya kazi. Katika dini, kuna watu wengi ambao wanaweza kutenda ukweli unaotendwa na mwanadamu wa Enzi ya Sheria. Hata hivyo, hawana amri za enzi mpya nao hawawezi kuzishika amri za enzi mpya. Wao huifuata njia ya zamani nao hubaki kama binadamu wa asili. Hawaambatani na namna mpya ya kazi nao hawawezi kuziona amri ya enzi mpya. Kimsingi, kazi ya Mungu haipo. Wao ni kama mtu aliyeshika ganda tupu la yai: Hakuna roho kama hakuna kifaranga ndani mwake. Tukizungumza kwa udhahiri, hakuna maisha. Watu kama hawa hawajaingia katika enzi mpya nao wamekawia nyuma kwa hatua nyingi. Kwa hiyo, ni bure kama watu wanao ukweli wa enzi ya miaka ya zamani lakini hawana amri za enzi mpya. Wengi wenu mnautenda ukweli wa wakati huu lakini hamzishiki amri za wakati huu. Hamtapata chochote, ukweli mnaoutenda utakuwa bure na bila maana naye Mungu hatausifu. Kuutenda ukweli lazima ufanyike kwa njia ambayo Roho Mtakatifu hufanya kazi leo; ni lazima ufanyike kwa kufuata sauti ya Mungu wa vitendo leo. Bila hii, kila kitu ni bure—kama vile kuchota maji na kikapu cha mianzi. Hii ndiyo maana halisi ya kutangazwa rasmi kwa amri za enzi mpya. Ikiwa watu wanapaswa kutii amri hizo, angalau kabisa wanafaa kumjua Mungu mwenye vitendo anayeonekana katika mwili bila kukanganyikiwa. Yaani, watu wanapaswa kuelewa kanuni za kutii sheria. Kutii sheria hakumaanishi kuzifuata kiholela ama bila mpangilio, bali kuzitii ukiwa na msingi, na lengo, na

kanuni. Kitu cha kwanza cha kufanikishwa ni maono yako kuwa dhahiri. Ikiwa unao uelewa wa kina wa kazi ya Roho Mtakatifu katika wakati wa sasa nawe uingie namna ya kazi ya leo, kwa kawaida utaona kiini cha kuziweka amri. Kama siku itakuja utakapoonza kiini cha amri za enzi mpya nawe utaweza kuzishika amri, basi wakati huo utakuwa umekamilika. Hii ndiyo maana ya kweli ya kuutenda ukweli na kuzishika amri. Ikiwa unaweza kuutenda ukweli au la inategemea jinsi unavyotambua kiini cha amri ya enzi mpya. Kazi ya Roho Mtakatifu itaonekana daima kwa mwanadamu naye Mungu itahitaji zaidi na zaidi kutoka kwa mwanadamu. Kwa hiyo, kweli ambazo mwanadamu huzitenda kwa kweli zitakuwa zaidi na kubwa zaidi nayo madhara ya kuzishika amri yatakuwa ya kushangaza zaidi. Kwa hiyo, ninyi mtautenda ukweli na kuzishika amri kwa wakati mmoja. Hakuna mtu atakayepuuza jambo hili. Hebu ukweli mpya na amri mpya zianze kwa wakati mmoja katika enzi hii mpya.

Unapaswa Kujua kuwa Mungu wa Vitendo Ni Mungu Mwenyewe

Je, unapaswa kujua nini kuhusu Mungu wa vitendo? Mungu wa vitendo Mwenyewe anajumuisha Roho, Nafsi, na Neno, na hii ndiyo maana ya kweli ya Mungu wa utendaji Mwenyewe. Kama unajua Nafsi pekee—kama unajua tabia na utu Wake—lakini hujui kazi ya Roho, au ambacho Roho hufanya katika mwili, na kuangazia Roho tu, na Neno, na kuomba mbele ya Roho, bila kujua kazi ya Roho wa Mungu katika Mungu wa vitendo, basi hii inadhihirisha kuwa humjui Mungu wa vitendo. Ufahamu wa Mungu wa vitendo unajumuisha kujua na kuyapitia maneno Yake, na kuelewa sheria na kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu, na jinsi Roho wa Mungu anavyofanya kazi katika mwili. Kwa hivyo, pia, inajumuisha kujua kwamba kila tendo la Mungu katika mwili linaongozwa na Roho, na kwamba maneno Anenayo ni maonyesho ya moja kwa moja ya Roho. Hivyo, ukitaka kumjua Mungu wa vitendo, lazima kimsingi ujue jinsi ambavyo Mungu hufanya kazi katika ubinadamu na katika uungu; hili, wakati ule ule, linahusu maonyesho ya Roho, ambayo watu wote hujihusisha nayo.

Ni nini kilichomo katika maonyesho ya Roho? Wakati mwingine Mungu hufanya kazi miongoni mwa ubinadamu, na wakati mwingine katika uungu—lakini kwa jumla, Roho anatawala katika pande zote mbili. Hata iwe ni roho gani ndani ya watu, hivyo ndivyo huwa maonyesho yao ya nje. Roho anafanya kazi kawaida, lakini kuna pande mbili za uelekezaji Wake kwa Roho: Upande mmoja ni kazi Yake kwa ubinadamu, na upande mwingine ni kupitia uungu. Unafaa kujua haya wazi wazi. Kazi ya Roho hubadilika kulingana na matukio: Wakati kazi Yake ya binadamu inahitajika, Roho anaielekeza kazi hii ya binadamu, na wakati kazi ya uungu inahitajika, uungu hujitokeza moja kwa moja kuifanya. Kwa sababu Mungu hufanya kazi katika mwili na kujionyesha katika mwili, Anafanya kazi katika ubinadamu na katika uungu. Kazi Yake

katika ubinadamu inaongozwa na Roho, na ili kuyaridhisha mahitaji ya kimwili ya watu, kuwezesha ushirikiano wao Naye, kuwafanya waone uhalisi na ukawaida wa Mungu, na kuwafanya waone kuwa Roho amekuja katika Mwili, na Yuko miongoni mwa wanadamu, Anaishi pamoja na wanadamu, na Hushirikiana na wanadamu. Kazi Yake ya uungu ni kwa ajili ya kuwapa watu uzima, na kuwaelekeza watu katika kila kitu kwa upande mzuri, na kubadili tabia za watu na kuwafanya waone kwa kweli kuonekana kwa Roho katika mwili. Kwa kiwango kikubwa, ukuaji katika maisha ya mwanadamu unapatikana moja kwa moja kupitia kazi ya Mungu na maneno katika uungu. Ikiwa tu watu wataikubali kazi ya Mungu ya uungu wataweza kubadili tabia zao, na hapo tu ndipo wataweza kushibishwa katika roho zao; ni ikiwa tu, ikiongezwa kwa hili, ndipo kutakuwa na kazi katika ubinadamu—uchungaji wa Mungu, usaidizi, na riziki kwa ubinadamu—ndipo matokeo ya kazi ya Mungu yanaweza kufanikishwa kikamilifu. Mungu wa vitendo Mwenyewe ambaye Anazungumziwa leo hufanya Kazi katika uungu na ubinadamu. Kupitia kwa kujitokeza kwa Mungu wa vitendo, kazi Yake ya kawaida ya binadamu na maisha na kazi Yake kamilifu ya uungu vinapatikana. Ubinadamu na uungu wake vimeungwa kuwa kitu kimoja, na kazi ya pande zote mbili inakamilishwa kupitia maneno; iwe katika ubinadamu au uungu, Ananena maneno. Mungu anapofanya Kazi katika ubinadamu, Anazungumza lugha ya ubinadamu, ili watu waweze kushiriki na kuelewa. Maneno Yake yanasemwa waziwazi, na ni rahisi kueleweka, kiasi kwamba yanaweza kutolewa kwa watu wote; bila ya kujali kuwa hawa watu wana ufahamu au hawajasoma vyema, wote wanaweza kupokea maneno ya Mungu. Kazi ya Mungu katika uungu vilevile inaweza kufanywa kupitia maneno, lakini imejawa na riziki, imejawa na uzima, haijatiwa dosari na mawazo ya mwanadamu, haihusishi mapenzi ya mwanadamu, na haina mipaka ya binadamu, iko nje ya mipaka ya ubinadamu wowote wa kawaida; vilevile, inafanywa katika mwili, lakini ni maonyesho ya moja kwa moja ya Roho. Kama watu wanaikubali kazi ya Mungu katika ubinadamu tu, basi watajiwekea mipaka katika upeo fulani, na hivyo milele watahitaji kushughulikiwa, kupogolewa, na kufundishwa nidhamu ili kwamba pawepo na mabadiliko kidogo ndani yao. Bila ya Kazi au uwepo wa Roho Mtakatifu, ingawa, watairudia mienendo yao ya awali; ni kupitia kazi ya uungu tu ndio haya maradhi na upungufu vitaweza kurekebishwa, hapo ndipo watu wanafanywa kuwa wakamilifu. Badala ya kushughulikia na kupogoa mara kwa mara, kinachohitajika ni matokeo mazuri, kwa kutumia maneno kufidia upungufu wote, kutumia maneno ili kufichua hali zote za watu, kutumia maneno kuyaelekeza maisha yao, kila matamshi yao, kila tendo lao, ili kuziweka wazi nia na motisha yao; hii ni kazi halisi ya Mungu wa vitendo. Na kwa hivyo, katika mwelekeo wako kwa Mungu wa vitendo unafaa kunyenyekeka mbele ya ubinadamu Wake, ukimkubali na kumtambua, na zaidi, unapaswa kukubali na kutii kazi ya uungu na maneno. Kuonekana kwa Mungu katika mwili kunamaanisha kuwa kazi yote na maneno ya Roho wa Mungu yanafanywa katika ubinadamu wake wa kawaida, na kupitia mwili Wake uliopatikana.

Kwa maneno mengine, Roho wa Mungu huelekeza kazi Yake ya ubinadamu na hutekeleza kazi Yake ya uungu katika mwili, na katika Mungu kupata mwili unaweza kuona kazi ya Mungu katika ubinadamu na kazi kamili ya uungu; huu ndio umuhimu wa utendaji hata zaidi wa kuonekana kwa Mungu wa vitendo katika mwili. Ukiweza kuliona hili wazi, utaweza kuhusisha sehemu zote za Mungu, na utaacha kuthamini sana kazi Yake ya uungu, na kuwa mwenye kupuuza sana kazi Yake katika ubinadamu, na hautazidi mipaka wala kupita njia za michepuo. Kwa jumla, maana ya Mungu wa vitendo ni kuwa kazi Yake ya ubinadamu na kazi Yake ya uungu, kama inavyoelekezwa na Roho, inaonyeshwa kupitia mwili Wake, ili watu waone kuwa Yeye ni wazi na mwenye kufanana na kiumbe chenye uhai, na ni halisi na wa hakika.

Kazi ya Roho wa Mungu katika ubinadamu ina awamu za mpito. Kwa kuwafanya ubinadamu wakamilifu, Anawawezesha ubinadamu Wake kupokea mwelekeo wa Roho, ambapo baadaye ubinadamu Wake unaweza kuyakimu na kuyaongoza makanisa. Hii ni aina moja ya maonyesho ya kazi ya kawaida ya Mungu. Hivyo, ukiweza kuona wazi kanuni za kazi ya Mungu katika ubinadamu, basi itakuwa vigumu kwako kuwa na dhana kuhusu kazi ya Mungu katika ubinadamu. Bila kujali kitu kingine chochote, Roho wa Mungu hawezi kukosea. Yuko sahihi, na Hana dosari; Hawezi kufanya kitu chochote kimakosa. Kazi ya uungu ni maonyesho ya moja kwa moja ya mapenzi ya Mungu, bila maingilio ya ubinadamu. Haipitii ukamilifu, ila inatoka moja kwa moja kwa Roho. Na bado, kufanya Kwake kazi katika uungu ni kwa sababu ya ubinadamu Wake wa kawaida; si miujiza, na kazi inaonekana kana kwamba imefanywa na mwanadamu wa kawaida; Kimsingi Mungu alitoka mbinguni kuja duniani ili kuonyesha maneno ya Mungu kupitia mwili, kukamilisha kazi ya Roho wa Mungu kwa kutumia mwili.

Ufahamu wa watu leo kuhusu Mungu wa vitendo bado unaegemea upande mmoja, na ufahamu wao kuhusu umuhimu wa kupata mwili bado ni mdogo sana. Kuhusu suala la mwili wa Mungu, watu huona kupitia katika kazi na maneno Yake kwamba Roho wa Mungu ana mengi, kwamba yeye ni tajiri. Lakini, hata hivyo, ushuhuda wa Mungu hatimaye hutoka kwa Roho wa Mungu: Anachokifanya Mungu katika Mwili, ni kanuni gani anatumia, anachokifanya katika ubinadamu, na anachokifanya katika uungu. Watu lazima wawe na ufahamu wa hili. Leo unaweza kumwabudu huyu mtu, lakini kwa hakika unamwabudu Roho. Hiki ndicho kiwango cha chini kabisa kinachopaswa kufahamiwa kuhusu ufahamu wa watu kuhusu Mungu aliyepata mwili: kujua kiini cha Roho kupitia kwa mwili, kujua kazi ya uungu ya Roho katika mwili na kazi ya wanadamu katika mwili, kukubali maneno yote ya Roho na matamshi katika mwili, na kuona jinsi Roho wa Mungu anauelekeza mwili na kudhihirisha uwezo Wake katika mwili. Hivi ni kusema kuwa, mwanadamu anapata kumjua Roho aliye mbinguni kupitia kwa mwili; kuonekana kwa Mungu wa vitendo Mwenyewe miongoni mwa wanadamu kumemwondoa Mungu asiye yakini kutoka katika dhana za wanadamu; ibada ya watu kwa Mungu wa vitendo

Mwenyewe imeongeza utiifu wao kwa Mungu; na kupitia kwa uungu wa kazi ya Roho wa Mungu katika Mwili, na kazi ya wanadamu katika miili, mwanadamu hupata ufunuo, na kuongozwa, na mabadiliko hupatikana katika tabia ya maisha yake. Hii tu ndiyo maana halisi ya ujio wa Roho katika mwili, kimsingi, ili kwamba watu waweze kushirikiana na Mungu, kumtegemea Mungu, na kuupata ufahamu wa Mungu.

Kwa kiasi kikubwa, ni mtazamo upi watu wanapaswa kuwa nao kuhusu Mungu wa vitendo? Unajua nini kuhusu kupata mwili, kuhusu kuonekana kwa Neno katika mwili, kuhusu kuonekana kwa Mungu katika mwili, na matendo ya Mungu wa vitendo? Mada kuu za kuzungumziwa leo ni zipi? Kupata mwili, ujio wa Neno katika mwili, kuonekana kwa Mungu katika mwili yote ni masuala ambayo ni lazima yaeleweke. Ni lazima mpate kuyaelewa haya masuala hatua kwa hatua na muwe na ufahamu ulio wazi kuyahusu katika uzoefu wenu wa maisha, kwa msingi wa kimo chenu na kwa msingi wa enzi. Mchakato ambamo watu huyapitia maneno ya Mungu ni sawa na mchakato ambamo wanafahamu kujitokeza kwa maneno ya Mungu katika mwili. Kadiri watu wanavyoyapitia maneno ya Mungu, ndivyo wanavyomjua Roho wa Mungu; kwa kuyapitia maneno ya Mungu, watu wanaelewa kanuni za kazi ya Roho na kupata kumjua Mungu wa vitendo Mwenyewe. Kwa hakika, Mungu akiwafanya watu wakamilifu na kuwachukua, Anawafanya wayajue matendo ya Mungu wa vitendo; Anatumia kazi ya Mungu wa vitendo kuwaonyesha watu umuhimu halisi wa kupata mwili, na kuwaonyesha kuwa Roho wa Mungu hakika ameonekana kwa mwanadamu. Watu wakichukuliwa na kufanywa wakamilifu na Mungu, maonyesho ya Mungu wa vitendo huwa amewashinda, maneno ya Mungu wa vitendo huwa yamewabadilisha, na kutoa uzima Wake ndani yao, kuwajaza na kile Alichu (iwe ni uwepo wake wa binadamu, au ule wa uungu), kuwajaza kwa kiini cha maneno Yake, na kuwafanya watu waishi kwa kudhihirisha maneno Yake. Mungu akiwapata watu, kimsingi Anafanya hivyo kwa kutumia maneno na matamko ya Mungu wa vitendo ili kuushughulikia upungufu wa watu, na kuhukumu na kufichua tabia zao za uasi, kuwafanya wapate wanachokihitaji, na kuwaonyesha kuwa Mungu yuko miongoni mwa wanadamu. Muhimu zaidi, kazi ifanywayo na Mungu wa vitendo ni kumwokoa kila mtu kutoka katika ushawishi wa Shetani, kuwatoa katika nchi ya uchafu, na kuziondoa tabia zao potovu. Umuhimu mkubwa zaidi wa watu kupatikana na Mungu wa vitendo ni kuwa na uwezo wa kumfanya Mungu wa vitendo kielelezo, na kuishi kulingana na ubinadamu wa kawaida, kuweza kutenda kulingana na maneno na mahitaji ya Mungu wa vitendo, bila upotofu au kuteleza, kutenda kama Asemavyo, na kuweza kufanikisha lolote Atakalo. Kwa njia hii, utakuwa umepatwa na Mungu. Ukipatwa na Mungu, hupati tu kazi ya Roho Mtakatifu; kidegesturi, unaweza kuzidisha mahitaji ya Mungu wa utendaji. Kuwa tu na kazi ya Roho Mtakatifu hakumaanishi kuwa una uzima. Cha muhimu ni kama unaweza kuishi kwa kudhihirisha mahitaji ya Mungu wa vitendo, ambayo inahusiana na kama unaweza kupatikana na

Mungu. Haya mambo ndiyo muhimu zaidi katika kazi ya Mungu wa vitendo katika mwili. Hivi ni kusema kuwa, Mungu analipata kundi la watu kwa kuonekana halisi na hakika katika mwili na kuwa wazi na mwenye kufanana na kiumbe chenye uhai, Akionekana na watu, hasa Akifanya kazi ya Roho katika mwili, na kwa kuwa kielelezo kwa watu wenye miili. Kimsingi, ujio wa Mungu katika mwili ni kuwawezesha watu kuona matendo halisi ya Mungu, kumfanya Roho asiye na umbo kuwa bayana katika mwili, na kuwapa watu fursa ya kumwona na kumgusa. Kwa njia hii, wanaokamilishwa Naye wataishi kwa kumfuata Yeye, watamfaidi na kuupendeza moyo Wake. Mungu angalinena kutoka mbinguni tu, na hakika asije duniani, basi bado watu hawangeweza kumjua, wangeweza tu kuyahubiri matendo ya Mungu kwa kutumia nadharia tupu, na hawangekuwa na maneno ya Mungu kama uhalisi. Mungu amekuja duniani kimsingi kuwa mfano na kielelezo kwa wale ambao wamepatwa na Mungu; ni kwa njia hii pekee ndio watu wanaweza kumjua Mungu kwa hakika, na kumgusa Mungu, na kumwona, na hapo ndipo wanaweza kupatikana na Mungu kwa kweli.

Kuuweka tu Ukweli Katika Matendo Ndiko Kuwa na Uhalisi

Kuwa na uwezo wa kuyaeleza maneno ya Mungu kwa uwazi haimaanishi kwamba wewe unaumiliki uhalisi—mambo si rahisi kama ulivyoweza kufikiria. Ikiwa unaumiliki uhalisi au la haina msingi kwa kile unachokisema, badala yake, inatokana na kile unachoishi kwa kudhihirisha. Wakati maneno ya Mungu yanakuwa maisha yako na kujionyesha kwako kwa asili, hili tu ndilo linalochukuliwa kama uhalisi, na hili tu ndilo linachukuliwa kama wewe kumiliki uelewa na kimo cha kweli. Lazima uwe na uwezo wa kuhimili uchunguzi kwa muda mrefu, na lazima uwe na uwezo wa kuishi kwa kudhihirisha sura ambayo inahitajika kwako na Mungu; isiwe mkao tu, lakini ni lazima ibubujike kwa kawaida kutoka ndani mwako. Hapo tu ndipo basi utakapokuwa na uhalisi kikweli, na ndipo tu basi utakapopata maisha. Wacha Nitumie mfano wa jaribio la watendaji huduma ambao kila mtu ana uzoefu nao. Mtu yeyote anaweza kuzungumzia nadharia zenye fahari sana kuhusu watendaji huduma, na kila mtu ana ufahamu unaofaa wa mada hii; wanazungumza juu yake na kila usemi unazidi ule wa awali, kana kwamba kuna mashindano. Hata hivyo, kama mwanadamu hajapitia jaribio kubwa, ni vigumu kusema ana ushahidi mzuri. Kwa ufupi, kuishi kwa kudhihirisha kwa mwanadamu bado kuna upungufu mwingi, na hii inatofautiana na uelewa wake. Kwa hiyo, bado hakijakuwa kimo halisi cha mwanadamu, na bado hayajakuwa maisha ya mwanadamu. Kwa sababu uelewa wa mwanadamu haujaletwa katika uhalisi, kimo chake bado ni kama ngome iliyojengwa kwenye mchanga, ikiyumbayumba na ikiwa karibu kuanguka. Mwanadamu anao uhalisi kidogo mno—ni vigumu kuupata uhalisi wowote katika mwanadamu. Kunao uhalisi kidogo mno unaobubujika kwa asili kutoka kwa mwanadamu na uhalisi wote katika maisha yake umelazimishwa, ndiyo maana nasema kwamba mwanadamu hamiliki uhalisi wowote. Usiweke hisa nyingi sana katika

wanadamu wakisema kwamba upendo wao wa Mungu haubadiliki kamwe—hiki tu ndicho kile wao husema kabla ya kukabiliwa na majaribu. Mara tu wanapokabiliwa na majaribu kwa ghafla, mambo ambayo wao hunena kwa mara nyingine tena hayalingani na uhalisi, na kwa mara nyingine yatathibitisha kwamba wanadamu hawana uhalisi. Inaweza kusemwa kwamba wakati wowote unapokumbana na mambo ambayo hayalingani na dhana zako nayo yanakuhitaji kujiweka kando, haya ni majaribu yako. Kabla mapenzi ya Mungu kufichuliwa, kuna mtihani mkali kwa kila mwanadamu, jaribio kubwa kwa kila mtu—je, waweza kuliona wazi jambo hili? Wakati Mungu anapotaka kuwajaribu wanadamu, Yeye daima huwaacha kufanya maamuzi yao kabla ya ukweli wa uhalisi kufichuliwa. Yaani wakati Mungu anamweka mwanadamu katika majaribu, kamwe Yeye hatakwambia ukweli, na hivyo ndivyo wanadamu wanaweza kufichuliwa. Hii ni njia mojawapo ambayo Mungu huifanya kazi yake, ili kuona kama unamwelewa Mungu wa leo, na ili kuona kama unaumiliki uhalisi wowote. Je, kweli wewe huna shaka yoyote kuhusu kazi ya Mungu? Je, utaweza kusimama imara wakati jaribio kuu linakuja? Ni nani anayethubutu kusema maneno kama vile “Nahakikisha hakutakuwa na matatizo”? Nani anayethubutu kusema maneno kama vile “Wengine wanaweza kuwa na mashaka, lakini Mimi sitakuwa na shaka kamwe”? Kama vile nyakati Petro alipitia majaribu—alikuwa siku zote akizungumza maneno makubwa kabla ukweli haujafichuliwa. Huu sio udhaifu wa kibinafsi wa kipekee kwa Petro; hii ni shida kubwa zaidi inayomkabili kila mwanadamu sasa. Kama ningetembelea maeneo kadhaa, au kama ningewatembelea ndugu na dada kadhaa, kuuangalia uelewa wenu wa kazi ya Mungu ya leo, hakika mngeweza kweli kuzungumza kuhusu mengi ya uelewa wenu, nayo ingeonekana kwamba ninyi hamna mashaka yoyote. Kama ningewauliza: “Je, kweli waweza kutabainisha kwamba kazi ya leo inatekelezwa na Mungu Mwenyewe? Bila shaka yoyote”? ungejibu bila shaka: “Bila shaka yoyote, ni kazi inayotekelezwa na Roho wa Mungu.” Mara tu unapojibu kwa namna hiyo, kwa hakika usingekuwa hata na chembe cha shaka na unaweza hata kuhisi starehe kubwa—unaweza kuhisi kuwa umepata uhalisi kiasi kidogo. Wale ambao mara nyingi huelewa mambo kwa njia hii ni wale ambao wanamiliki uhalisi kidogo zaidi; kadri mtu anavyodhani kwamba amelipata, ndivyo atakavyokosa uwezo wa kusimama imara katika majaribio. Ole wao walio na kiburi na wenye maringo, na ole wao wasio na maarifa ya wao wenyewe. Watu kama hawa ni hodari katika kuzungumza ilhali huendelea vibaya zaidi katika matendo yao. Wakati kuna dalili ndogo zaidi ya matatizo, watu hawa wataanza kuwa na mashaka na mawazo ya kukata tamaa huingia akilini mwao. Hawana umiliki wa uhalisi wowote; yote waliyo nayo ni nadharia zenye fahari zaidi kuliko zile za dini, bila ya hali halisi ambazo Mungu anadai sasa. Nachukizwa zaidi na wale wanaosema kuhusu nadharia tu nao hawana uhalisi. Wao kufanya kilio kikubwa zaidi wanapoitenda kazi yao, lakini wao husambaratika punde tu wanapokabiliwa na uhalisi. Je, si inaonyesha kwamba watu hawa hawana uhalisi? Haijalishi jinsi upepo na mawimbi yalivyo kali, kama unaweza kubaki umesimama bila hata

dalili ya shaka kuingia mawazoni mwako, na unaweza kusimama imara na usiwe kati hali ya kukana hata kama hakuna mtu mwingine aliyebaki, basi hili linachukuliwa kama wewe kuwa na uelewa wa kweli na wewe kuwa na umiliki wa uhalisi. Ukifuata njia yoyote ambayo upepo unavuma, ukiwafuata walio wengi na kujifunza kusema yale ambayo wengine wanasema, haijalishi jinsi gani unavyosema mambo hayo vizuri, sio thibitisho kwamba unao umiliki wa uhalisi. Kwa hiyo, napendekeza kwamba usiwe na haraka ya kupiga kelele kwa maneno matupu. Je, unaijua kazi ambayo Mungu ataitekeleza? Usitende kama Petro mwingine usije ukajiletea aibu na usiweze tena kutembea bila haya—hii haimfaidi mtu yeyote. Wanadamu wengi hawana kimo cha kweli. Mungu ametekeleza kazi kubwa sana lakini hajafanya uhalisi kuwajia watu; kwa kuwa sahihi zaidi, Mungu hajawahi kumwadibu yeyote binafsi. Baadhi ya watu wamefichuliwa na majaribio kama haya, na minyiri yao ya dhambi ikitambaa nje zaidi na zaidi, wakifikiri kwamba ni rahisi kumhadaa Mungu, wanaweza kumchukulia Mungu kwa kutojali, na kufanya chochote wanachotaka. Kwa kuwa hawawezi hata kustahimili majaribu ya aina hii, kadri majaribio yenye changamoto yasivyowezezekana, na uhalisi pia hauwezekani. Je, si hii ni kujaribu kumpumbaza Mungu? Kuwa na uhalisi si kitu ambacho kinaweza kubuniwa, na wala si kitu ambacho unaweza kukipata kutokana na maarifa yako kukihusu. Unalingana na kimo chako cha ukweli, na unalingana na kama unao uwezo wa kuhimili majaribu yote. Je, unaelewa sasa?

Masharti ya Mungu kwa wanadamu siyo tu kuweza kuzungumza kuhusu uhalisi. Je, si hiyo itakuwa rahisi sana? Kwa nini basi Mungu anazungumza kuhusu kuingia katika maisha? Kwa nini Anaongea kuhusu mabadiliko? Kama mtu ana uwezo wa mazungumzo matupu tu kuhusu uhalisi, mabadiliko katika tabia yangeweza kupatikana? Kulifunza kundi la wanajeshi wazuri wa ufalme sio sawa na kuwafunza wanadamu ambao wanaweza tu kiongea kuhusu uhalisi au watu ambao hujigamba tu, bali ni kuwafunza wanadamu ambao wanajivunia tu, lakini wanadamu ambao wanaweza kuishi kwa kudhihirisha maneno ya Mungu wakati wote, ambao ni wagumu bila kujali vikwazo wanavyokumbana navyo, na wanaoishi kwa mujibu wa maneno ya Mungu wakati wote, na hawarudi kwa ulimwengu. Huu ndio uhalisi ambao Mungu anauzungumzia, nayo ni matakwa ya Mungu kwa binadamu. Kwa hiyo, usiuone uhalisi ulionenwa na Mungu kama rahisi sana. Kupata nuru tu kwa Roho Mtakatifu sio sawa na kuumiliki uhalisi: Hiki sicho kimo cha wanadamu, lakini neema ya Mungu, nayo haihusishi mafanikio yoyote ya wanadamu. Kila mwanadamu ni lazima ayavumilie mateso ya Petro, na hata zaidi aumiliki utukufu wa Petro, ambao ndio watu huishi kwa kudhihirisha baada ya kupata kazi ya Mungu. Hii tu ndiyo inaweza kuitwa uhalisi. Usidhani kwamba utamiliki uhalisi kwa sababu unaweza kuzungumza kuhusu uhalisi. Huu ni uongo, huu haulingani na mapenzi ya Mungu, na hauna maana halisi. Usiseme mambo kama haya katika siku zijazo—komesha misemo kama hii! Wale wote walio na uelewa wa uongo wa maneno ya Mungu ni makafiri. Hawana maarifa yoyote halisi, sembuse kimo

chochote halisi; wao ni watu wenye kujigamba bila ya uhalisi. Hiyo ni, wale wote wanaoishi nje ya dutu ya maneno ya Mungu ni makafiri. Wale wanaoonekana kuwa makafiri na wanadamu ni wanyama mbele za Mungu, na wale wanaoonekana kuwa makafiri na Mungu ni wale ambao hawana maneno ya Mungu kama maisha yao. Kwa hiyo, wale ambao hawana uhalisi wa maneno ya Mungu nao wanashindwa kuishi kwa kudhihirisha maneno ya Mungu ni makafiri. Nia ya Mungu ni kufanya iwe kwamba kila mmoja anaishi kwa kudhihirisha uhalisi wa maneno ya Mungu. Sio tu kwamba kila mtu anaweza kuzungumza kuhusu uhalisi, lakini muhimu zaidi, kwamba kila mmoja anaweza kuishi kwa kudhihirisha uhalisi wa maneno ya Mungu. Uhalisi ambao mwanadamu anautambua ni wa juu juu sana, hauna thamani, hauwezi kutimiza mapenzi ya Mungu, ni duni sana, hata haustahili kutajwa, una upungufu sana, na uko mbali sana na kiwango cha mahitaji ya Mungu. Kila mmoja wenu atapitia ukaguzi mkuu ili kuona ni nani kati yenu anayejua tu kuzungumza kuhusu uelewa wake lakini hawezi kuonyesha njia, na kuona ni nani kati yenu ni taka bure. Kumbuka hili katika siku zijazo! Usizungumze kuhusu uelewa mtupu—zungumza tu kuhusu njia ya utendaji, na kuhusu uhalisi. Geuka kutoka maarifa halisi hadi kwenye vitendo halisi, na kisha geuka kutoka kutenda hadi kuishi kwa kudhihirisha uhalisi. Usiwahutubie wengine, na usizungumze kuhusu maarifa ya ukweli. Kama uelewa wako ni njia, basi unaweza kuuachilia; kama si njia, basi tafadhali nyamaza, na uache kuongea. Kile unachosema ni bure. Ni baadhi tu ya maneno ya uelewa ya kumpumbaza Mungu na kuwafanya wengine wakuonee wivu. Si hilo ni lengo lako? Je, hii si kuwachezea wengine kimakusudi? Je, kunayo thamani yoyote katika hili? Zungumza tu kuhusu uelewa baada ya kuwa na uzoefu kuuhusu, na kisha hutakuwa unajisifu tena. La sivyo wewe ni mtu tu ambaye anasema maneno yenye kiburi. Huwezi hata kuyashinda mambo mengi au kuasi dhidi ya mwili wako wenyewe katika uzoefu wako halisi, siku zote ukifanya chochote unachoelekezwa kukifanya kwa tamaa zako, sio kwa kuyaridhisha mapenzi ya Mungu, lakini bado unayo nyongo ya kuzungumzia uelewa wa kinadharia—huna haya! Bado unayo nyongo ya kuzungumza kuhusu uelewa wako wa maneno ya Mungu—wewe ni fidhuli jinsi gani! Kuhutubu na kujisifu kumekuwa asili yako, na umekuwa na desturi ya kufanya hili. Unalijua sana kila wakati unapotaka kuzungumza, unalifanya kwa ustadi na bila kufikiria, nawe unajiingiza katika mapambo inapokuja wakati wa kutenda. Je, si hii ni kuwapumbaza wengine? Unaweza kuwapumbaza wanadamu, lakini Mungu hawezi kupumbazwa. Wanadamu hawajui na hawana utambuzi, lakini Mungu anatilia maanani masuala hayo, naye hatakusaza. Ndugu na dada zako wanaweza kukutetea, wakiusifu uelewa wako, wakipendezwa nawe, lakini ikiwa huna uhalisi, Roho Mtakatifu hatakusaza. Pengine Mungu wa matendo hatazikaripia dosari zako, lakini Roho wa Mungu hataweka makini yoyote kwako, na hiyo itatosha wewe kuvumilia. Je, unaamini hili? Zungumza zaidi kuhusu uhalisi wa utendaji; Je, umeshasahau tayari? Zungumza zaidi kuhusu njia za kiutendaji; Je, ushasahau tayari? “Zungumza kwa uchache kuhusu nadharia za fahari au mazungumzo mazuri yasiyo na

maana, na ni bora kuanza mazoezi kuanzia sasa.” Je, umesahau maneno haya? Je, huelewi yoyote haya? Je, hauna uelewa wa mapenzi ya Mungu?

Kuijua Kazi ya Mungu Leo

Kuijua kazi ya Mungu katika nyakati hizi, kwa sehemu kubwa, ni kujua kile ambacho ni huduma kuu ya Mungu katika mwili katika siku za mwisho, na kile ambacho Amekuja kufanya duniani. Hapo mwanzoni Nimesema katika maneno Yangu kwamba Mungu Amekuja duniani (katika siku za mwisho) ili kuweka mfano kabla Hajaondoka. Ni kwa jinsi gani Mungu Ameuweka mfano huu? Kwa kuzungumza maneno, kwa kufanya kazi na kuzungumza katika nchi nzima. Hii ni kazi ya Mungu wakati wa siku za mwisho; Anazungumza tu ili dunia iwe ulimwengu wa maneno, ili kila mtu awe amepewa na kutiwa nuru maneno Yake, na ili roho ya mwanadamu iamshwe na aweze kuona vizuri kuhusu maono yake. Wakati wa siku za mwisho, Mungu katika mwili Amekuja duniani hasa kwa ajili ya kuzungumza maneno. Yesu Alipokuja, Alieneza injili ya ufalme wa mbinguni, na Akatimiza kazi ya wokovu wa msalaba. Alihitimisha Enzi ya Sheria, na Akakomesha mambo yote ya kale. Ujio wa Yesu ulihitimisha Enzi ya Sheria na kuanzisha Enzi ya Neema. Ujio wa Mungu katika mwili wa siku za mwisho umehitimisha Enzi ya Neema. Amekuja hasa kwa ajili ya kuzungumza maneno Yake, kutumia maneno ili kumfanya mwanadamu mkamilifu, kumwangazia na kumpa nuru mwanadamu, na kumwondoa Mungu asiye yakini katika moyo wa mwanadamu. Hii sio hatua ya kazi ambayo Yesu Aliifanya Alipokuja. Yesu Alipokuja, Alifanya miujiza mingi, Aliponya wagonjwa na kutoa mapepo, na Alifanya kazi ya wokovu ya msalaba. Na matokeo yake ni kwamba, katika dhana za mwanadamu, mwanadamu anaamini kwamba hivi ndivyo Mungu Anapaswa kuwa. Maana Yesu Alipokuja, hakufanya kazi ya kuondoa taswira ya Mungu asiye yakini moyoni mwa mwanadamu; Alipokuja, Alisulubishwa, Aliponya wagonjwa na kutoa mapepo, na Alieneza injili ya ufalme wa mbinguni. Kwa upande mmoja, Mungu katika mwili katika siku za mwisho Anaondoa nafasi iliyochukuliwa na Mungu asiye yakini katika dhana za mwanadamu, ili taswira ya Mungu asiye yakini isiwepo kabisa katika moyo wa mwanadamu. Kwa kutumia maneno Yake halisi na kazi Yake halisi, Anazunguka katika nchi zote, na kazi Anayoifanya miongoni mwa wanadamu ni halisi kabisa na ya kawaida, kana kwamba mwanadamu anakuja kujua uhalisia wa Mungu na Mungu asiye yakini Anapoteza nafasi Yake moyoni mwake. Kwa upande mwingine, Mungu Anatumia maneno yaliyozungumzwa na mwili Wake ili kumfanya mwanadamu mkamilifu, na kukamilisha vitu vyote. Hii ndiyo kazi ambayo Mungu Ataikamilisha wakati wa siku za mwisho.

Kile mnachopaswa kujua:

1. Kazi ya Mungu si ya kimiujiza, na hampaswi kuhifadhi dhana juu yake.

2. Mnapaswa kuelewa kazi kuu ambayo Mungu katika mwili Amekuja kufanya wakati huu.

Hakuja kuponya wagonjwa, au kutoa mapepo, au kufanya miujiza, na Hajakuja kueneza injili ya toba, au kumpatia mwanadamu ukombozi. Hiyo ni kwa sababu Yesu Amekwishafanya kazi hii, na Mungu Harudii kazi ile ile. Leo, Mungu Amekuja kuhitimisha Enzi ya Neema, na kuzitupilia mbali desturi zote za Enzi ya Neema. Mungu wa vitendo Amekuja hasa kuonyesha kuwa Yeye ni halisi. Yesu Alipokuja Alizungumza maneno machache; hasa Alionyesha miujiza, Akafanya ishara na maajabu, na Akaponya wagonjwa na kutoa mapepo, au wakati mwingine Alizungumza unabii ili kumshawishi mwanadamu, na kumfanya mwanadamu aone kwamba ni kweli Alikuwa Mungu, na Alikuwa Mungu Asiyepelelea. Hatimaye, Akakamilisha kazi ya msalaba. Mungu wa leo Haonyeshi ishara na maajabu, wala Haponyi wagonjwa na kutoa mapepo. Yesu Alipokuja, kazi Aliyoifanya iliwakilisha upande mmoja wa Mungu, lakini wakati huu Mungu Amekuja kufanya hatua ya kazi ambayo imetazamiwa, maana Mungu Harudii kazi ile ile; ni Mungu ambaye siku zote ni mpya na Hawezi kuzeeka kamwe, na hivyo yale yote unayoyaona leo ni maneno na kazi ya Mungu wa vitendo.

Mungu katika mwili wa siku za mwisho Amekuja hasa kwa ajili ya kuzungumza maneno Yake, ili kuelezea yale yote ambayo ni ya lazima katika maisha ya mwanadamu, kuonyesha yale ambayo mwanadamu anapaswa kuingia kwayo, kumwonesha mwanadamu matendo ya Mungu, na kumwonesha mwanadamu hekima, uweza na uajabu wa Mungu. Kupitia njia nyingi ambazo Mungu Anazungumza, mwanadamu anatazama ukuu wa Mungu, aidha, unyenyekevu na usiri wa Mungu. Mwanadamu anatazama kwamba Mungu ni mkuu, lakini ni mnyenyekevu na msiri, na Anaweza kuwa mdogo kuliko vitu vyote. Baadhi ya maneno Yake yanazungumzwa moja kwa moja kutoka kwa mtazamo wa Roho, baadhi ya hayo moja kwa moja kutoka katika mtazamo wa mwanadamu, na baadhi kutoka katika mtazamo wa nafsi ya tatu. Katika hili, inaweza kuonekana kwamba namna ya kazi ya Mungu inatofautiana kwa kiasi kikubwa na ni kwa njia ya maneno ndipo Anamruhusu mwanadamu kuiona. Kazi ya Mungu wakati wa siku za mwisho ni ya kawaida na halisi, na hivyo kundi la watu wa siku za mwisho wanakumbwa na majaribu makubwa kuliko yote. Kwa sababu ya ukawaida na uhalisia wa Mungu, watu wote wameingia katika majaribu hayo; kwamba mwanadamu ameingia katika majaribu ya Mungu ni kwa sababu ya ukawaida na uhalisia wa Mungu. Wakati wa enzi ya Yesu, hakukuwa na dhana au majaribu. Kwa sababu kazi kubwa iliyofanywa na Yesu ilikuwa ni kulingana na dhana za mwanadamu, watu walimfuata, na hawakuwa na dhana juu Yake. Majaribu ya leo ni makubwa sana ambayo yamewahi kukabiliwa na mwanadamu, na inaposemwa kwamba watu hawa wametoka katika dhiki kuu, hii ndiyo dhiki inayoongelewa. Leo, Mungu Ananena ili kusababisha imani, upendo, ustahimilivu na utii kwa watu hawa. Maneno yaliyozungumzwa na Mungu katika mwili wa siku za mwisho ni kutokana na hulka ya asili ya mwanadamu, kulingana na tabia ya mwanadamu, na

kulingana na kile ambacho mwanadamu anapaswa kuingia kwacho leo. Maneno ni halisi na ya kawaida: Hazungumzi juu ya kesho, wala Haangalii nyuma, jana; Anazungumza kile tu ambacho kinapaswa kuingiwa kwacho, kuwekwa katika vitendo, na kueleweka leo. Kama, wakati wa zama hizi, kutatokea mtu mwenye uwezo wa kuonyesha ishara na maajabu, na kutoa mapepo, kuponya wagonjwa, na kufanya miujiza mingi, na kama mtu huyu anadai kwamba yeye ni Yesu ambaye amekuja, basi hii itakuwa ni ghushi ya roho wachafu, na kumuiga Yesu. Kumbuka hili! Mungu Harudii kazi ile ile. Hatua ya kazi ya Yesu tayari imekwisha kamilika, na Mungu Hataichukua tena hatua hiyo ya kazi. Kazi ya Mungu haipatani na dhana za mwanadamu; kwa mfano, Agano la Kale lilitabiri juu ya ujio wa Masihi, lakini ilikuwa dhahiri kwamba Yesu Alikuwa, hivyo itakuwa makosa kwa Masihi mwingine kuja tena. Yesu tayari Amekwishakuja mara moja, na yatakuwa ni makosa ikiwa Yesu Atakuja tena wakati huu. Kuna jina moja kwa kila enzi, na kila jina linaeleza sifa ya enzi. Katika dhana za mwanadamu, Mungu ni lazima siku zote Aonyeshe ishara na maajabu, ni lazima siku zote Aponye wagonjwa na kutoa mapepo, na siku zote ni lazima Awe tu kama Yesu, lakini Mungu wakati huu Hayupo kama hivyo kabisa. Ikiwa, wakati wa siku za mwisho, Mungu bado Angeonyesha ishara na maajabu, na bado Angetoa mapepo na kuponya wagonjwa—kama Angefanya vilevile ambavyo Yesu Alifanya—basi Mungu Angekuwa Anarudia kazi ile ile, na kazi ya Yesu isingekuwa na maana au thamani yoyote. Hivyo, Mungu Anatekeleza hatua moja ya kazi katika kila enzi. Mara tu kila hatua ya kazi Yake inapokamilika, baada ya muda mfupi inaigizwa na roho wachafu, na baada ya Shetani kuanza kufuata nyayo za Mungu, Mungu Anabadilisha na kutumia mbinu nyingine. Mara Mungu Anapokamilisha hatua ya kazi Yake, inaigizwa na roho wachafu. Lazima muelewe vizuri hili. Kwa nini kazi ya Mungu leo ni tofauti na kazi ya Yesu? Kwa nini Mungu leo Haonyeshi ishara na maajabu, Hatoi mapepo, na Haponyi wagonjwa? Ikiwa kazi ya Yesu ingekuwa sawa na kazi iliyoifanywa katika Enzi ya Sheria, je, Angekuwa Amemwakilisha Mungu wa Enzi ya Neema? Je, Yeye Angekuwa Amemaliza kazi ya msalaba? Ikiwa, kama katika Enzi ya Sheria, Yesu Angeingia hekaluni na kuitunza Sabato, basi Asingeteswa na mtu yeyote na Angekumbatiwa na wote. Kama ingekuwa hivyo, je, Angesulubiwa? Je, Angekuwa Amemaliza kazi ya ukombozi? Je, ingekuwa na maana gani ikiwa Mungu katika mwili wa siku za mwisho Angeonyesha ishara na maajabu kama Yesu? Ikiwa tu Mungu Atafanya sehemu nyingine ya kazi Yake wakati wa siku za mwisho, kazi inayowakilisha sehemu ya mpango wa usimamizi Wake, ndipo mwanadamu anaweza kupata maarifa ya kina ya Mungu, na baada ya hapo tu ndipo mpango wa usimamizi wa Mungu unaweza kukamilika.

Wakati wa siku za mwisho, Mungu Amekuja mahususi kwa ajili ya kuzungumza maneno Yake. Anazungumza kutokana na mtazamo wa Roho, kutokana na mtazamo wa mwanadamu, na kutokana na mtazamo wa nafsi ya tatu; Anazungumza kwa namna tofauti, Akitumia njia moja

kwa kipindi fulani, na Anatumia njia za kuzungumza ili kubadilisha dhana za mwanadamu na kuondoa taswira ya Mungu yakini katika moyo wa mwanadamu. Hii ndiyo kazi kuu iliyofanywa na Mungu. Kwa sababu mwanadamu anaamini kwamba Mungu Amekuja kuponya wagonjwa, kutoa mapepo, kufanya miujiza, na kumpatia mwanadamu baraka za vitu, Mungu Anatekeleza hatua hii ya kazi—kazi ya kuadibu na hukumu—ili kuweza kuondoa mambo hayo kutoka katika dhana za mwanadamu, ili mwanadamu aweze kuuelewa uhalisia na ukawaida wa Mungu, na ili kwamba taswira ya Yesu iweze kuondolewa moyoni mwake na kuwekwa taswira mpya ya Mungu. Mara tu taswira ya Mungu ndani ya mwanadamu inapozeeka, basi inakuwa sanamu. Yesu alipokuja na kutekeleza hatua hii ya kazi, Hakuwakilisha Mungu kikamilifu. Alifanya baadhi ya ishara na maajabu, Alizungumza maneno kadhaa, na hatimaye Akasulubishwa, na Aliwakilisha upande mmoja wa Mungu. Hakuweza kuwakilisha yale yote ambayo ni ya Mungu, bali Alimwakilisha Mungu katika kufanya upande mmoja wa kazi ya Mungu. Hiyo ni kwa sababu Mungu ni mkuu, na ni wa ajabu sana, na Haeleweki, na kwa sababu Mungu Anafanya upande mmoja tu wa kazi Yake katika kila enzi. Kazi inayofanywa na Mungu katika enzi hii ni hasa ya kutoa maneno kwa ajili ya uzima wa mwanadamu; kufunuliwa kwa tabia potovu ya mwanadamu na kiini cha asili ya mwanadamu; na uondoaji wa fikira za kidini, fikra za kinjozi, mitazamo iliyopitwa na wakati, vilevile maarifa na utamaduni wa mwanadamu. Hii ni lazima iwekwe wazi na kusafishwa kupitia maneno ya Mungu. Katika siku za mwisho, Mungu Anatumia maneno na siyo ishara na maajabu ili kumfanya mwanadamu kuwa mkamilifu. Anatumia maneno Yake kumweka wazi mwanadamu, kumhukumu mwanadamu, kumwadibu mwanadamu, na kumkamilisha mwanadamu, ili katika maneno ya Mungu, mwanadamu aje kuona hekima na wema wa Mungu, na aje kuelewa tabia ya Mungu, ili kupitia maneno ya Mungu, mwanadamu aone matendo ya Mungu. Wakati wa Enzi ya Sheria, Yehova Alimwongoza Musa kutoka Misri kwa maneno Yake, na Akazungumza maneno fulani kwa Wanaisraeli; wakati huo, sehemu ya matendo ya Mungu yaliwekwa wazi, lakini kwa sababu ubora wa tabia ya mwanadamu ulikuwa finyu na hakuna kitu chochote ambacho kingeweza kufanya maarifa yake kukamilika, Mungu Aliendelea kuzungumza na kufanya kazi. Wakati wa Enzi ya Neema, mwanadamu aliweza kuona tena sehemu ya matendo ya Mungu. Yesu Aliweza kuonyesha ishara na maajabu, kuponya wagonjwa na kutoa mapepo, na kusulubishwa, siku tatu baadaye. Akafufuka na Akawatokea watu Akiwa katika mwili. Kumhusu Mungu, mwanadamu hakujua chochote zaidi ya hiki. Mwanadamu anajua tu kile ambacho Mungu Amemwonyesha, na kama Mungu Asingewonyesha chochote zaidi kwa mwanadamu, basi hicho kingekuwa kiwango cha mwanadamu kumwekea mipaka Mungu. Hivyo, Mungu Anaendelea kufanya kazi, ili maarifa ya mwanadamu juu Yake yaweze kuwa ya kina zaidi, na ili taratibu aweze kuijua hulka ya Mungu. Katika siku za mwisho, Mungu anatumia maneno yake kumkamilisha mwanadamu. Tabia yako iliyoharibika imewekwa wazi kwa maneno ya Mungu, na dhana zako za kidini

zinaondolewa na uhalisia wa Mungu. Mungu katika mwili wa siku za mwisho Amekuja hasa kwa ajili ya kutimiza maneno haya kwamba “Neno Lafanyika kuwa mwili, Neno Lakuwa mwili, na Neno Laonekana katika mwili,” na kama huna maarifa ya kina kuhusu hili, basi hutaweza kusimama imara. Wakati wa siku za mwisho, kimsingi Mungu Anakusudia kukamilisha hatua ya kazi ambayo kwayo Neno Anaonekana katika mwili, na hii ni sehemu moja ya mpango wa usimamizi wa Mungu. Hivyo, maarifa yenu yanapaswa kuwa wazi; bila kujali namna ambavyo Mungu Anafanya kazi, Mungu Hamruhusu mwanadamu kumwekea mipaka. Ikiwa Mungu Asingefanya kazi hii wakati wa siku za mwisho, basi maarifa ya mwanadamu juu Yake yasingeweza kwenda popote. Ungeweza kujua tu kwamba Mungu Anaweza kusulubiwa na Anaweza kuiangamiza Sodoma, na kwamba Yesu Anaweza kufufuliwa kutoka katika wafu na kumtokea Petro.... Lakini usingeweza kusema kwamba maneno ya Mungu yanaweza kutimiza yote, na yanaweza kumshinda mwanadamu. Ni kwa njia tu ya kupitia uzoefu wa maneno ya Mungu ndipo unaweza kuzungumza juu ya maarifa hayo, na kadri unapopitia uzoefu wa kazi ya Mungu zaidi, ndivyo maarifa yako yanavyokuwa ya kina zaidi kumhusu Yeye. Ni baada ya hapo tu ndipo utaacha kumwekea Mungu mipaka ndani ya dhana zako binafsi. Mwanadamu anakuja kumjua Mungu kwa kupitia kazi Yake, na hakuna njia nyingine sahihi ya kumjua Mungu. Leo, kuna watu wengi ambao hawafanyi chochote bali wanasubiri kuona ishara na maajabu na wakati wa maafa makubwa. Je, unamwamini Mungu, au unaamini katika maafa makubwa? Maafa makubwa yatakapofika muda utakuwa umeisha, na ikiwa Mungu hataleta maafa makubwa, basi Atakuwa si Mungu? Je, unaamini ishara na maajabu, au unamwamini Mungu Mwenyewe? Yesu Hakuonyesha ishara na maajabu wakati Alipobezwa na wengine; je, Hakuwa Mungu? Je, unaamini ishara na maajabu, au unaamini katika hulka ya Mungu? Mitazamo ya mwanadamu kuhusu imani kwa Mungu ni makosa! Yehova Alizungumza maneno mengi wakati wa Enzi ya Sheria, lakini hata leo baadhi yake bado hayajitimizwa. Je, unaweza kusema kwamba Yehova Hakuwa Mungu?

Leo, inapaswa kueleweka kwenu wote kwamba, katika siku za mwisho, ni kwa kiasi kikubwa ukweli wa “Neno linakuwa mwili” ambao unakamilishwa na Mungu. Kupitia kazi yake halisi duniani, Anafanya mwanadamu kumfahamu, na kushirikiana Naye, na kuona matendo Yake halisi. Anamsababisha mwanadamu kuona kwa wazi kwamba Yeye Anaweza kuonyesha ishara na maajabu na pia kuna nyakati ambapo Hawezi kufanya hivyo, na hii inategemea enzi. Kutokana na hili unaweza kuona kwamba Mungu sio kwamba Hawezi kuonyesha ishara na maajabu, lakini badala yake Anabadilisha kufanya kazi Kwake kulingana na kazi Yake, na kulingana na enzi. Katika hatua ya sasa ya kazi, Haonyeshi ishara na maajabu; kuonyesha kwake baadhi ya ishara na maajabu katika enzi ya Yesu, ilikuwa ni kwa sababu kazi Yake katika enzi hiyo ilikuwa tofauti. Mungu Hafanyi kazi hiyo leo, na baadhi ya watu wanaamini Hana uwezo

wa kuonyesha ishara na maajabu, au wanafikiri kwamba kama Haonyeshi ishara na maajabu, basi Yeye si Mungu. Hii sio hoja ya uwongo? Mungu Anaweza kuonyesha ishara na maajabu, lakini Anafanya kazi katika enzi tofauti, na hivyo Hafanyi kazi hiyo. Kwa kuwa hii ni enzi tofauti, na kwa kuwa hii ni hatua tofauti ya kazi ya Mungu, matendo yaliyowekwa wazi na Mungu pia ni tofauti. Imani ya mwanadamu kwa Mungu sio imani katika ishara na maajabu, wala imani katika miujiza, bali ni imani katika kazi Yake halisi wakati wa enzi mpya. Mwanadamu anamjua Mungu kupitia namna ambavyo Mungu Anafanya kazi, na maarifa haya yanamfanya mwanadamu amwamini Mungu, ambavyo ni kusema, imani katika kazi na matendo ya Mungu. Katika hatua hii ya kazi, Mungu Anazungumza hasa. Usisubiri kuona ishara na maajabu; hutayaona! Maana hukuzaliwa katika Enzi ya Neema. Kama ungezaliwa katika Enzi ya Neema, ungeweza kuona ishara na maajabu, lakini umezaliwa katika siku za mwisho, na hivyo unaweza kuona tu uhalisia na ukawaida wa Mungu. Usitarajie kumwona Yesu wa kimiujiza wakati wa siku za mwisho. Unaweza kumwona tu Mungu katika mwili wa vitendo, Ambaye si tofauti na mwanadamu yeyote wa kawaida. Katika kila enzi, Mungu Anaweka wazi matendo mbalimbali. Katika kila enzi Anaweka wazi sehemu ya matendo ya Mungu, na kazi ya kila enzi inawakilisha sehemu moja ya tabia ya Mungu, na inawakilisha sehemu moja ya matendo ya Mungu. Matendo Anayoyaweka wazi yanatofautiana na enzi ambayo kwayo Anafanya kazi, lakini yote yanampatia mwanadamu maarifa ya Mungu ambayo ni ya kina, imani kwa Mungu ambayo ni yenye kuhusika na mambo halisi sana, na ambayo ni ya kweli zaidi. Mwanadamu anamwamini Mungu kwa sababu ya matendo yote ya Mungu, na kwa sababu Mungu ni wa ajabu ni mkuu sana, kwa sababu Yeye ni mwenyezi, na ambaye Hapimiki kina. Ikiwa unamwamini Mungu kwa kuwa Anaweza kufanya ishara na maajabu na Anaweza kuponya wagonjwa na kuwatoa mapepo, basi mtazamo wako si sahihi, na baadhi ya watu watakwambia, “Je, pepo wachafu pia hawawezi kufanya mambo hayo?” Je, hii sio kuielewa vibaya taswira ya Mungu kwa kuilinganisha na taswira ya Shetani? Leo, imani ya mwanadamu kwa Mungu ni kwa sababu ya matendo Yake mengi na kiasi kikubwa cha kazi Anachofanya na njia nyingi ambazo kwazo Ananena. Mungu Anatumia matamshi yake kumshinda mwanadamu na kumfanya mkamilifu. Mwanadamu anamwamini Mungu, kwa sababu ya matendo Yake mengi, na si kwa sababu Anaweza kuonyesha ishara na maajabu, na wanadamu wanamwelewa tu kwa sababu wanaona matendo Yake, Ni kwa kujua tu matendo halisi ya Mungu, namna Anavyofanya kazi, njia ambazo Anaonyesha hekima Yake, vile Anavyozungumza, na jinsi Anavyomfanya mwanadamu kuwa mkamilifu—ni kwa kujua tu vipengele hivi—ndipo unaweza kufahamu uhalisia wa Mungu na kuelewa tabia Yake, kujua kile Anachopenda, kile Anachochukia, namna Anavyomfanyia kazi mwanadamu. Kwa kuelewa yale ambayo Mungu Anayapenda na Asiyoyapenda, unaweza kutofautisha kati ya kile ambacho ni chanya na kile ambacho ni hasi, na kupitia maarifa yako juu ya Mungu kunakuwa na maendeleo katika maisha yako. Kwa ufupi unapaswa kuwa na maarifa

ya kazi ya Mungu, na unapaswa kuweka sahihi mitazamo yako kuhusu kuwa na imani kwa Mungu.

Je, Kazi ya Mungu Ni Rahisi Kama Vile Mwanadamu Anavyodhania?

Kama mtu anayemwamini Mungu, inakupasa kuelewa kuwa, leo, katika kupokea kazi ya Mungu nyakati za mwisho na kazi yote ya mpango wa Mungu ndani yako, umepokea utukufu mkuu na wokovu wa Mungu kabisa. Kazi yote ya Mungu ulimwengu mzima imelenga watu wa kikundi hiki. Amejitolea kwa nguvu Zake zote na kutoa vyote kwa ajili yako; Amekurejesha na kukupa kazi yote ya Roho ulimwenguni kote. Ndiyo sababu Nasema kuwa wewe una bahati. Zaidi ya hayo, Amehamisha utukufu wake kutoka kwa Israeli, watu wake wateule, hadi kwako, ili kufanya kusudio lake lijidhihirishe kwenu kama kundi. Kwa hiyo, ninyi ndio mtakaopokea urithi wa Mungu, na hata zaidi warithi wa utukufu wa Mungu. Pengine utayakumbuka maneno haya: “Kwa kuwa huzuni yetu nyepesi, ambayo ni ya muda mdogo pekee, inatufanyia utukufu mkubwa na wa daima ambao unazidi kuwa mkuu kabisa.” Zamani, mlisikia msemu huu, lakini hakuna aliyelewa maana kamili ya maneno yale. Leo, unajua vyema umuhimu wa maneno yale. Maneno haya ndiyo yatakayotimizwa na Mungu katika enzi za mwisho. Yatatimia kwa wale walioteswa na joka kuu jekundu katika sehemu linakoishi. Joka kuu jekundu humtesa Mungu na ni adui wa Mungu, kwa hiyo katika nchi hii, wanaomwamini Mungu wanateswa na kudhihakiwa. Ndiyo sababu maneno haya yatakuja kuwa kweli kwenu nyie kundi la watu. Kazi inapotekelezwa katika nchi inayompinga Mungu, kazi Yake yote inakabiliwa na vizuizi vya kupita kiasi, na mengi ya maneno Yake hayawezi kutimizwa katika wakati ufaao: ndiyo maana, watu husafishwa kwa ajili ya neno la Mungu. Hiki pia ni kipengele cha mateso. Ni vigumu kabisa kwa Mungu kutekeleza kazi yake katika nchi yenye joka kuu jekundu, lakini ni kupitia ugumu huu ndipo Mungu Hupiga hatua katika kazi Yake ili kudhihirisha hekima Yake na matendo Yake ya ajabu. Mungu Huchukua fursa hii kuwakamilisha watu hawa wa kikundi hiki. Kwa ajili ya mateso ya watu, tabia yao na hulka ya kishetani ya watu katika nchi hii najisi, Mungu Anafanya kazi Yake ya kutakasa na ushindi, ili, kutokana na hili, apokee utukufu na kuwapata wale wote wanaoshuhudia matendo Yake. Huu ndio umuhimu wa kujitoa kwa Mungu kwa ajili ya kikundi hiki cha watu. Ina maana kuwa Mungu hufanya kazi ya ushindi kupitia wale wanaompinga. Kufanya vile tu ndiko kunaweza kudhihirisha nguvu kuu za Mungu. Kwa maneno mengine, ni wale tu walio katika nchi najisi ndiyo wanaostahili kuurithi utukufu wa Mungu na ni hili tu ambalo litafanya nguvu kuu za Mungu kuwa maarufu. Ndiyo maana Nasema kuwa utukufu wa Mungu unapatikana katika nchi najisi na kwa wale wanaoishi humo. Haya ndiyo mapenzi ya Mungu. Hii ni kama tu ilivyokuwa katika kazi ya Yesu; Angetukuzwa tu kati ya

Mafarisayo waliomdhihaki. Isingelikuwa mateso na usaliti wa Yuda, Yesu asingelidhihakiwa na kudharauliwa, na hata zaidi kusulubiwa, na hivyo asingelipokea utukufu. Kila mara Mungu Anapofanya kazi katika wakati fulani na kila mara anapofanya kazi Yake kwa kupitia mwili, huwa Anapokea utukufu na papo hapo huwapata Anaotaka kuwapata. Huu ndio mpango wa kazi ya Mungu na hivi ndivyo anavyosimamia kazi Yake.

Katika mpango wa Mungu wa miaka elfu kadhaa, kazi inayofanywa ndani ya mwili ni katika sehemu mbili: Kwanza ni kazi ya kusulubiwa, ambayo kwayo anatukuzwa; nyingine ni kazi ya ushindi na ukamilifu katika nyakati za mwisho, ambayo kwayo pia Atapokea utukufu. Huu ni usimamizi wa Mungu. Hivyo basi, usichukulie kazi ya Mungu au agizo Lake kwako kuwa rahisi sana. Ninyi ndio warithi wa uzito wa milele wa utukufu wa Mungu, hili lilituliwa na Mungu. Katika sehemu hizo mbili za utukufu wa Mungu, moja inafichuliwa ndani yako; ukamilifu wa sehemu moja ya utukufu Wake umepewa ili uwe urithi wako. Huku ndiko kutukuzwa kutoka kwa Mungu na mpango wake uliopangwa kitambo. Kutokana na ukuu wa kazi alioifanya Mungu katika nchi ambako joka kuu jekundu linaishi, kazi kama hii, ikipelekwa katika sehemu nyingine, ingezaa tunda zuri kitambo na ingekubaliwa na mwanadamu kwa urahisi. Na kazi kama hii ingekuwa rahisi sana kukubaliwa na viongozi wa dini wa Magharibi wanaomwamini Mungu, kwani kazi ya Yesu ni kama kielelezo. Ndio maana Hawezi kutekeleza hatua hii ya kazi ya utukufu mahali pengine; yaani, kwa kuwa kuna uungaji mkono kwa watu wote na utambulisho wa mataifa yote, hamna mahali ambapo utukufu wa Mungu unaweza “kupumzikia.” Na huu ndio umuhimu wa kipekee wa hatua hii ya kazi katika nchi hii. Kati yenu, hamna mtu mmoja anayepokea ulinzi wa sheria; badala yake, unaadhibiwa na sheria, na ugumu mkubwa zaidi ni kuwa hapana mtu anayekuelewa, awe ni jamaa yako, wazazi wako, marafiki wako, ama watendakazi wenzako. Hakuna anayekuelewa. Mungu “Anapokukataa,” hapana uwezekano wako kuendelea kuishi duniani. Hata hivyo, watu hawawezi kumwacha Mungu; huu ndio umuhimu wa ushindi wa Mungu kwa watu, na huu ni utukufu wa Mungu. Kile ambacho umerithi wakati huu, kimepiku walichorithi mitume na manabii na ni kikuu zaidi kuliko alichopokea Musa na Petro. Baraka haziwezi zikapokewa kwa siku moja au mbili; sharti zipatikane kwa kujitolea kwingi. Yaani, lazima uwe na upendo uliosafishwa, imani kuu, na ukweli mwingi ambao Mungu Anakuagiza uufikie; zaidi ya hayo, sharti uelekeze uso wako kwa haki wala usikubali kushindwa, na lazima uwe na upendo usiofikia kikomo kwa ajili ya Mungu. Azimio linahitajika kutoka kwako, na vilevile mabadiliko katika tabia ya maisha yako. Upotovu wako lazima utibiwe, na lazima ukubali mipango ya Mungu pasipo kulalamika, na hata uwe mtiifu hadi kifo. Hicho ndicho unachopaswa kutimiza. Hili ndilo lengo la mwisho la kazi ya Mungu, na matakwa ya Mungu kwa watu wa kundi hili. Anapokukarimia mengi, anakutaka wewe badala yake na kukufanyia matakwa yanayokufaa. Kwa hiyo, kazi yote ya Mungu haipo

bila sababu, na kutokana na hili inaonekana ni kwa nini Mungu kila mara hufanya kazi ya hali ya juu na yenye mahitaji makali. Ndiyo maana unafaa kujawa na imani katika Mungu. Kwa ufupi, kazi yote ya Mungu hufanywa kwa ajili yako, ili kwamba uweze kupokea urithi Wake. Hii sio kwa ajili ya utukufu wa Mungu bali ni kwa ajili ya wokovu wako na kufanya kundi hili la watu walioteswa na nchi najisi kuwa wakamilifu. Sharti uelewe mapenzi ya Mungu. Kwa hiyo Nawahimiza wale wote wasiojua, wasio na hisia na ufahamu: Usimjaribu Mungu wala kumpinga tena. Mungu Ameshavumilia mateso yote ambayo mwanadamu hajaweza kupitia, na hapo awali Ameteseka na kudhihakiwa kwa niaba ya mwanadamu. Je, nini kingine ambacho huwezi kukiachilia? Je, ni nini muhimu zaidi kuliko mapenzi ya Mungu? Ni nini zaidi kuliko upendo wa Mungu? Ni kazi ambayo ina ugumu mara mbili zaidi kwa Mungu kufanya katika nchi najisi. Ikiwa mtu atatenda dhambi kimakusudi na akifahamu, kazi ya Mungu itaendelezwa kwa muda mrefu zaidi. Katika tukio lolote, hili silo pendeleo la yeyote wala si la maana kwa yeyote. Mungu Hafungwi na wakati; kazi Yake na utukufu Wake huchukua mstari wa mbele. Kwa hiyo, hata ikichukua muda mrefu, Hataacha kutoa dhabihu yoyote ikiwa ni kazi Yake. Hii ndiyo silika ya Mungu: Hatapumzika hadi pale kazi Yake itakapokamilika. Ni pale tu ambapo wakati unapowadia na anapokea sehemu ya pili ya utukufu wake ndipo kazi Yake itakapokwisha. Mungu Asipokamilisha sehemu ya pili ya utukufu wake ulimwenguni, Siku Yake haitawadia, mkono wake hauwezi kuwaachilia wateule wake, utukufu wake hautashuka juu ya Israeli na mpango wake kamwe hauwezi kukamilishwa. Mnapaswa kuona mapenzi ya Mungu na kuona kwamba kazi ya Mungu si rahisi kama ilivyokuwa katika kuumba mbingu na nchi na vyote vilivyomo. Hiyo ni kwa sababu kazi ya leo ni mabadiliko ya wale waliopotoshwa, wale walio baridi kwa kiasi kikubwa zaidi, ni ili kuwatakasa wale walioumbwa lakini wakashughulikiwa na Shetani. Si uumbaji wa Adamu na Hawa, sembuse kuumba mwanga, ama aina yote ya mimea na wanyama. Kazi Yake sasa ni kutakasa wote waliopotoshwa na Shetani ili kwamba wamrejeele, wawe miliki Yake na wawe utukufu wake. Kazi kama ile si rahisi jinsi mwanadamu anavyofikiria kuhusu kuumbwa kwa mbingu na nchi na vilivyomo, wala si sawa na kumkemea Shetani aende katika shimo lisilo na mwisho, kama anayodhanja mwanadamu. Bali, ni kumbadilisha mtu, kubadili kilicho hasi kuwa chanya na kufanya kuwa miliki Yake ambacho si chake. Huu ndio undani wa hadithi ya hatua hii ya kazi ya Mungu. Lazima ufahamu wala usirahisishe mambo. Kazi ya Mungu ni tofauti na kazi nyingine. Uzuri wake hauwezi kutambuliwa na akili za mwanadamu wala hekima Yake kupatikana vile. Wakati wa hatua hii ya kazi Yake, Mungu Haumbi kila kitu wala kuharibu kila kitu. Bali, Anabadilisha viumbe vyote na kutakasa vyote vilivyonajisiwa na Shetani. Kwa hiyo, Mungu Atanzisha kazi kuu, na huu ndio umuhimu wa kazi ya Mungu. Baada ya kusoma maandishi haya, je, unaamini kuwa kazi ya Mungu ni rahisi vile?

Unapaswa Kuishi kwa Ajili ya Ukweli kwa Maana Unamwamini Mungu

Tatizo la kawaida lililo miongoni mwa binadamu wote ni kwamba wao huuelewa ukweli lakini hawawezi kuuweka katika matendo. Sababu moja ni kwamba binadamu hana nia ya kulipa gharama, na sababu nyingine ni kwamba utambuzi wa mwanadamu ni duni mno; hawezi kuona zaidi ya ugumu mwingi ulio katika hali halisi ya maisha na hajui jinsi ya kutenda kwa njia inayofaa. Kwa vile mtu ana tajriba ndogo sana, mwenye uwezo wa chini, mwenye ufahamu mdogo wa ukweli, yeye hawezi kutatua matatizo yanayomkabili maishani. Anaweza tu kupiga domo kuhusu imani yake kwa Mungu, ilhali hawezi kumhusisha Mungu katika maisha yake ya kila siku. Hii ni kusema, Mungu ni Mungu, na maisha ni maisha, kama kwamba binadamu hana uhusiano na Mungu katika maisha yake. Hayo ndiyo binadamu wote wanayaamini. Aina hii ya imani kwa Mungu haitaruhusu binadamu kupatwa na kukamilishwa Naye kwa uhakika. Kwa kweli, si kwamba neno la Mungu ni pungufu, badala yake uwezo wa binadamu wa kupokea neno Lake ni duni mno. Inaweza kusemwa karibu binadamu wote hutenda kulingana na nia za Mungu. Badala yake, imani yao kwa Mungu ni kwa mujibu wa nia zao wenyewe, fikra za kidini zilizowekwa, na desturi. Ni wachache wanaopitia mabadiliko baada ya kulikubali neno la Mungu na kuanza kutenda kwa mujibu wa mapenzi Yake. Badala yake, wanaendelea katika imani yao potovu. Wakati mwanadamu anaanza kuamini katika Mungu, anafanya hivyo kwa kuzingatia sheria za kawaida za dini, na anaishi na kuhusiana na wengine kwa misingi ya falsafa yake ya kuishi. Hivyo ndivyo ilivyo kwa watu tisa kati ya kila watu kumi. Ni wachache sana wanaounda mpango mwingine na kuanza mwanzo mpya baada ya kuanza kumwamini Mungu. Hakuna anayeona au kuweka katika vitendo neno la Mungu kama ukweli.

Chukua imani katika Yesu, kwa mfano. Kama mtu alikuwa mwanafunzi katika imani au alikuwa wa imani hiyo kwa muda mrefu, wote walitumia vipaji vyovyote walivyokuwa navyo na kuonyesha ujuzi wowote waliokuwa nao. Mwanadamu aliongeza tu “imani katika Mungu,” maneno haya matatu, katika maisha yake ya kawaida, bado hayakufanya mabadiliko katika tabia yake, na imani yao kwa Mungu haikukua hata kidogo. Ukimbizaji wa mwanadamu wa swala hili haukuwa baridi wala moto. Hakusema kwamba hakuamini, lakini pia hakujitoa kikamilifu kwa Mungu. Hakuwahi kumpenda Mungu kwa kweli wala kumtii Mungu. Imani yake kwa Mungu ilikuwa halali na ya kujifanya, na aligeuka na akapuuza na wala hakuwa na bidii kwa kutenda imani yake. Aliendelea katika hali kama hiyo ya kuchanganyikiwa tangu mwanzo hadi wakati wake wa kufa. Ni nini maana ya hili? Leo, lazima uwe katika njia sahihi kwani unaamini katika Mungu wa vitendo. Kwa kuwa una imani katika Mungu, hupaswi tu kutafuta baraka, lakini pia kutafuta kumpenda Mungu na kumjua Mungu. Kupitia kwa kupata nuru kutoka Kwake na

harakati yako mwenyewe, unaweza kula na kunywa neno Lake, kukuza ufahamu wa kweli kuhusu Mungu, na kuwa na upendo wa kweli kwa Mungu unaotoka moyoni mwako. Kwa maneno mengine, upendo wako kwa Mungu ni wa kweli zaidi, ambapo hakuna yeyote anayeweza kuharibu au kukuzuia kuonyesha upendo wako Kwake. Basi uko kwa njia ya kweli ya imani kwa Mungu. Inathibitisha kwamba wewe unamilikiwa na Mungu, kwani moyo wako umemilikiwa na Mungu na wala huwezi kumilikiwa na kitu kingine. Kutokana na tajriba yako, malipo uliyolipa, na kazi ya Mungu, wewe una uwezo wa kuendeleza upendo usioamriwa kwa Mungu. Kisha unawekwa huru kutoka kwa ushawishi wa Shetani na kuishi katika mwanga wa neno la Mungu. Ni wakati tu ambao umekuwa huru kutoka kwa ushawishi wa giza ndipo unaweza kuchukuliwa kuwa umempata Mungu. Katika imani yako kwa Mungu, lazima utafute lengo hili. Huu ni wajibu wa kila mmoja wenu. Hakuna anayelazimika kutosheka na mambo jinsi yalivyo. Hamuwezi kuwa na fikira aina mbili kwa kazi ya Mungu au uichukulie kwa wepesi. Mnapaswa kumfikiria Mungu katika mambo yako yote na wakati wote, na kufanya mambo yote kwa ajili yake. Na wakati mnasema au kufanya mambo, mnapaswa kutilia maanani maslahi ya nyumba ya Mungu kwanza. Ni hii tu ndio inayolingana na mapenzi ya Mungu.

Kosa kubwa sana la binadamu kuwa na imani katika Mungu ni kwamba imani yake ni ya maneno tu, na Mungu hayupo popote katika maisha yake ya utendaji. Watu wote, kwa kweli, wanaamini kuwepo kwa Mungu, lakini Mungu si sehemu ya maisha yao ya kila siku. Maombi mengi kwa Mungu hutoka katika kinywa cha mtu, lakini Mungu amepewa nafasi ndogo sana katika moyo wake, na hivyo Mungu humjaribu binadamu tena na tena. Kwa vile mtu ni mchafu, Mungu hana budi ila kumjaribu mtu, ili aweze kuona aibu na kisha aje kujitambua mwenyewe katika majaribu. La sivyo, mwanadamu atageuka mwana wa malaika mkuu, na kuzidi kuwa mpotovu. Wakati wa imani ya mtu katika Mungu, nia nyingi na malengo ya kibinafsi hutupwa mbali anavyotakaswa na Mungu bila kukoma. La sivyo, hakuna mwanadamu anayeweza kutumiwa na Mungu, na Mungu hana njia ya kufanya ndani ya mtu kazi anayopaswa kufanya. Mungu kwanza humtakasa mwanadamu. Katika mchakato huu, mtu anaweza kuja kujijua mwenyewe na Mungu huenda akambadilisha mwanadamu. Ni baada ya haya ndipo Mungu anaweza kuyashughulikia maisha ya mwanadamu, na kwa njia hii pekee ndio moyo wa binadamu unaweza kumgeukia Mungu kwa ukamilifu. Kwa hivyo, kumwamini Mungu si rahisi jinsi mwanadamu anaweza kuona. Mungu anavyoona, ukiwa tu na ufahamu lakini huna neno Lake kama uhai; ikiwa wewe unazingatia tu maarifa yako mwenyewe lakini huwezi kutenda ukweli au kuishi kwa kudhihirisha neno la Mungu, basi hii ni dhihirisho kwamba huna moyo wa upendo kwa Mungu, na inaonyesha kwamba moyo wako si mali ya Mungu. Kuja kumjua Mungu kwa kumwamini; hili ndilo lengo la mwisho na ambalo mwanadamu atatafuta. Lazima ufanye juhudi ya kuishi kwa kudhihirisha maneno ya Mungu ili yaweze kuonekana katika matendo

yako. Kama unayo maarifa ya mafundisho ya dini pekee, basi imani yako kwa Mungu itakuwa kazi bure. Kama wewe utatenda pia na kuishi kwa kudhihirisha neno Lake basi imani yako inaweza kuchukuliwa kuwa kamili na kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu. Katika njia hii, wanadamu wengi wanaweza kusema wana maarifa mengi, lakini katika wakati wao wa kufa, macho yao hujawa machozi, nao hujichukia wenyewe kwa kuharibu maisha yao yote na kuishi maisha yasiyo na mazao hadi uzeeni. Wanaelewa tu mafundisho lakini hawawezi kutia ukweli katika vitendo na kushuhudia kwa Mungu, badala yake wakikimbia huku na kule, wakiwa na kazi kama nyuki; mara wanapochungulia kaburi wao hatimaye huona kwamba hawana ushuhuda wa kweli, kwamba hawamjui Mungu kamwe. Je, si huku ni kuchelewa mno? Kwa nini usichukue nafasi hii na kufuatilia ukweli unaoupenda? Kwa nini usubiri hadi kesho? Iwapo katika maisha huwezi kuteseka kwa ajili ya ukweli au kutafuta kuupata, inaweza kuwa kwamba unataka kujuta katika saa yako ya kufa? Ikiwa hivyo, basi kwa nini umwamini Mungu? Kwa kweli, kuna mambo mengi ambayo mtu, iwapo ataweka juhudi kidogo tu, anaweza kuweka ukweli katika vitendo na hivyo kumridhisha Mungu. Moyo wa binadamu daima umepagawa na mapepo na kwa hivyo hawezi kutenda mambo kwa ajili ya Mungu. Badala yake, yeye daima yumo katika safari ya huku na kule kwa sababu ya mwili, na hafaidiki na chochote mwishowe. Ni kwa sababu hizi ndio mtu hupata matatizo ya mara kwa mara na mateso. Je, haya sio mateso ya Shetani? Je, huu sio ufisadi wa mwili? Hufai kumdanganya Mungu kwa maneno ya mdomo. Badala yake, lazima uchukue hatua inayoonekana. Usijidanganye; ni nini maana katika hilo? Ni faida gani utakayopata kutokana na kuishi kwa ajili ya mwili wako na kufanya bidii kwa ajili ya umaarufu na mali ya dunia?

Ngurumo Saba Zatoa Sauti—Zikitabiri Kuwa Injili ya Ufalme Itaenea Kote Ulimwenguni

Mimi Naeneza kazi Yangu katika nchi za Mataifa. Utukufu Wangu unamulika kotekote ulimwenguni; mapenzi Yangu yamo katika watu wa nyota-nyota-nukta-nukta, wote wakiongozwa kwa mkono Wangu na kufanya kazi ambayo Nimewapa. Kuanzia wakati huu kuendelea, Nimeingia katika enzi mpya, kuwaleta watu wote katika ulimwengu mwingine. Niliporudi katika “nchi Yangu,” Nilianza sehemu nyingine tena ya kazi katika mpango Wangu wa asili, ili mwanadamu aje kunijua zaidi. Nauchukua ulimwengu katika ukamilifu wake na kuona kwamba^[a] ni wakati muafaka wa kazi Yangu, kwa hiyo Naharakisha mbele na nyuma kufanya kazi Yangu mpya ndani ya mwanadamu. Hii ni enzi mpya, hata hivyo, na Nimeleta kazi mpya ili Niwachukue watu wapya wengi zaidi katika enzi mpya na kuachana na wengi wa wale Nitakaowaondoa. Katika taifa la joka kubwa jekundu, Nimetekeleza hatua ya kazi isiyoeleweka kwa wanadamu, kuwafanya kuyumba katika upepo, ambapo baadaye wengi wanabebwa kwa siri

na upepo unaovuma. Kweli, huu ni “uwanja wa kupura” Ninaotaka kuusafisha; ni kile Ninachotamani na pia ni mpango Wangu. Kwa maana wengi waovu wameingia ndani kimya wakati Niko kazini, lakini Sina haraka ya kuwafukuza. Badala yake, Nitawatawanya wakati utakapofika. Ni baada ya hapo tu ndipo Nitakuwa chemchemi ya uzima, kuwakubalia wanaonipenda kweli wapokee kutoka Kwangu tunda la mtini na harufu ya yungiyungi. Katika nchi ambako Shetani huishi, nchi ya vumbi, hakuna dhahabu safi iliyobaki, ila ni mchanga tu, na kwa hiyo, Nikikabiliwa na hali hizi, Nafanya hatua hiyo ya kazi. Lazima ujue kwamba Ninachopata ni dhahabu safi, iliyosafishwa, wala si mchanga. Ni jinsi gani waovu wanaweza kubaki katika nyumba Yangu? Ninawezaje kuruhusu Mbweha kuwa vimelea ndani ya paradiso Yangu? Natumia kila mbinu inayoweza kufikiriwa kuvifukuza vitu hivi. Kabla ya mapenzi Yangu kufichuliwa, hakuna anayefahamu Ninachotaka kufanya. Nikichukua fursa hii, Ninawafukuza wale waovu, na wanalazimika kuondoka machoni Pangu. Hili ndilo Mimi huwafanyia waovu, lakini bado kutakuwa na siku ya wao kunifanyia huduma. Hamu ya watu kupata baraka ni kubwa mno; Kwa hivyo Ninageuza mwili Wangu na kuonyesha uso Wangu wa utukufu kwa watu wa Mataifa, ili watu wote waishi katika dunia yao wenyewe na kujihukumu, huku Naendelea kusema maneno ambayo Napaswa kuyasema na kuwaruzuku wanadamu wanachohitaji. Wakati wanadamu wanapata fahamu, Nitakuwa Nimeeneza kazi Yangu kitambo. Kisha Nitawaonyesha wanadamu mapenzi Yangu, na kuanza sehemu ya pili ya kazi Yangu juu ya wanadamu, kuwaruhusu watu wote wanifuata kwa karibu ili waambatane na kazi Yangu, na kuwaruhusu watu kufanya kila wawezalo kutekeleza nami kazi Ninayopaswa kufanya.

Hakuna aliye na imani kwamba atauona utukufu Wangu, na Mimi simlazimishi, badala yake Nauondoa utukufu Wangu kutoka miongoni mwa wanadamu na kuupeleka kwa ulimwengu mwingine. Wakati watu watatubu tena, basi Nitauchukua utukufu Wangu na Nitaonyesha kwa wengi wa wale wanaoamini. Hii ni kanuni ambayo Mimi hufuata katika kazi Yangu. Kwa maana kuna wakati ambapo utukufu Wangu unaondoka Kanaani, na pia kuna wakati ambapo utukufu Wangu unawaacha waliochaguliwa. Zaidi ya hayo, kuna wakati ambapo utukufu Wangu unaiacha dunia nzima, kuisababisha kuwa hafifu na kuitumbukiza katika giza. Hata nchi ya Kanaani haitaona mwanga wa jua; wanadamu wote watapoteza imani yao, lakini hakuna hata mmoja anayeweza kuiacha nchi ya Kanaani ya kupendeza. Ninapopita katika mbingu na nchi mpya tu ndipo Ninachukua sehemu nyingine ya utukufu Wangu na kuifichua kwanza katika nchi ya Kanaani, Nikisababisha nuru kuiangazia dunia nzima, iliyozama katika giza totoro la usiku, ili kuruhusu dunia nzima kuja kwa nuru hiyo. Wacha watu wote duniani kote waje kupata nguvu kutoka kwa nuru, kuruhusu utukufu Wangu uongezeke na kuonekana upya kwa kila taifa. Wacha binadamu wote utambue kwamba Nilikuja zamani katika ulimwengu wa wanadamu na Nilileta utukufu Wangu kutoka Israeli hadi Mashariki zamani; kwani utukufu Wangu unang’aa kutoka

Mashariki, ambako uliletwa kutoka Enzi ya Neema hadi leo. Lakini Nilitokea Israeli na kutoka huko Nikawasili Mashariki. Wakati nuru ya Mashariki inapong'aa polepole tu ndipo giza kote duniani litaanza kugeuka na kuwa nuru, na hapo tu ndipo mwanadamu atatambua kwamba Nilishatoka Israeli zamani na Nimeanza kuchomoza upya Mashariki. Niliwahi kushuka Israeli na baadaye Niliondoka kutoka huko, Siwezi tena kuzaliwa Israeli kwa mara nyingine, kwa kuwa kazi Yangu inauongoza ulimwengu mzima na, zaidi ya hilo, umeme unamulika moja kwa moja kutoka Mashariki kwenda Magharibi. Hii ndiyo sababu Nimeshuka Mashariki na kuwaletea watu wa Mashariki Kanaani. Ningependa kuwaleta watu kutoka dunia nzima waje katika nchi ya Kanaani, na kwa hiyo Naendelea kutoa maneno Yangu katika nchi ya Kanaani ili kuudhibiti ulimwengu mzima. Kwa wakati huu, hakuna nuru katika dunia nzima isipokuwa katika Kanaani, na watu wote wamehatarishwa na njaa na baridi. Niliipa Israeli utukufu Wangu kisha Nikauchukua na baadaye Nikawaleta Waisraeli Mashariki, na vilevile binadamu wote Mashariki. Nimewaleta wote kwenye nuru ili waweze kuungana tena nayo, na kushirikiana na nuru, na wasilazimike kuitafuta tena. Nitawaacha wote wanaotafuta waone nuru tena na kuuona utukufu Niliokuwa nao katika Israeli; Nitawaacha waone kwamba tayari Nimeshuka juu ya wingu jeupe miongoni mwa wanadamu, kuwaacha waone mawingu mengi meupe na vishada vingi vya matunda, na, zaidi ya hayo, Nitawaacha wamwone Yehova Mungu wa Israeli. Nitawaacha waone Mkuu wa Wayahudi, Masihi aliyengojewa kwa hamu, na kuonekana kamili kwa Mimi niliyeteswa na wafalme kotekote katika enzi. Nitafanya kazi katika ulimwengu mzima na Nitatekeleza kazi kubwa, Nikifichua utukufu Wangu wote na matendo Yangu yote kwa mwanadamu katika siku za mwisho. Nitaonyesha uso Wangu uliojaa utukufu kwa wale ambao wameningoja kwa miaka mingi, kwa wale ambao wametamani kuniona Nikija juu ya wingu jeupe, kwa Israeli ambayo imengojwa Nionekane kwa mara nyingine, na kwa wanadamu wote wanaonitesa, ili wote wajue kwamba Niliuchukua utukufu Wangu zamani na kuuleta Mashariki, Ili usiwe katika Uyahudi tena. Kwani siku za mwisho tayari zimewadia!

Kotekote katika ulimwengu Ninafanya kazi Yangu, na katika Mashariki, mashambulio ya radi yanapiga bila kukoma, yakiyatingisha mataifa yote na madhehebu. Ni sauti Yangu ndiyo imewaleta watu katika wakati wa sasa. Nitawasababisha watu wote kushindwa na sauti Yangu, kuingia katika mkondo huu, na kunyenyekea mbele Yangu, kwa maana Nilijirudishia utukufu Wangu kutoka duniani kote zamani na Nikautoa upya Mashariki. Ni nani asiyetamani kuuona utukufu Wangu? Ni nani asiyesubiri kwa hamu kurudi Kwangu? Ni nani asiye na kiu cha kuonekana Kwangu tena? Ni nani asiyetamani kuona kupendeza Kwangu? Ni nani hangetaka kuja kwenye nuru? Ni nani hangeuona utajiri wa Kanaani? Ni nani hangoji kwa hamu kurudi kwa Mkombozi? Ni nani asiyempenda kwa dhati Mwenyezi Mkuu? Sauti Yangu itaenea kotekote duniani; Ningependa, kuwazungumzia maneno mengi zaidi wateule wangu,

Nikiwatazama. Kama radi yenye nguvu inayotingisha milima na mito, Nanena maneno Yangu kwa ulimwengu wote na kwa wanadamu. Hivyo maneno yaliyo kinywani Mwangu yamekuwa hazina ya mwanadamu, na watu wote wanayahifadhi maneno Yangu kwa upendo mkubwa. Umeme wa radi unaangaza kutoka Mashariki mpaka Magharibi. Maneno Yangu ni kiasi kwamba mwanadamu huchukia kuyaacha na pia huyaona kama yasiyoeleweka, lakini zaidi ya yote mwanadamu huyafurahia. Wanadamu wote wana uchangamfu na furaha, wakasherehekea kuja Kwangu, kana kwamba mtoto mchanga amezaliwa hivi karibuni. Kwa sauti Yangu, nitawaleta wanadamu wote mbele Yangu. Tangu hapo, Nitaingia rasmi katika jamii ya wanadamu ili waje kuniabudu. Kwa utukufu Ninaoutoa na maneno yaliyo kinywani Mwangu, Nitawafanya watu wote kuja mbele Yangu na kuona kwamba umeme unaangaza kutoka Mashariki na kwamba Mimi pia Nimeshuka kwenye “Mlima wa Mizeituni” wa Mashariki. Wataona kwamba Mimi tayari Nimekuwa duniani kwa muda mrefu, sio kama Mwana wa Wayahudi tena lakini kama Umeme wa Mashariki. Kwani Nimeshafufuka kitambo, na Nimeondoka miongoni mwa wanadamu, na kisha Nimeonekana tena miongoni mwa wanadamu Nikiwa na utukufu. Mimi ndiye Niliyeabudiwa enzi nyingi kabla ya wakati huu, na pia Mimi ni “mtoto mchanga” Aliyeachwa na Israeli enzi nyingi kabla ya wakati huu. Zaidi ya hayo, Mimi ndiye Mwenyezi Mungu mwenye utukufu wote wa enzi hii! Hebu wote waje mbele ya kiti Changu cha enzi ili waone uso Wangu mtukufu, wasikie sauti Yangu, na kuangalia matendo Yangu. Huu ndio ukamilifu wa mapenzi Yangu; ni mwisho na kilele cha mpango Wangu, na vilevile madhumuni ya usimamizi Wangu. Hebu kila taifa liniabudu Mimi, kila ulimi unikiri Mimi, kila mtu aniamini Mimi, na watu wote wawe chini Yangu!

Tanbihi:

a. Maandishi ya asili hayana kauli “kuona kwamba.”

Tofauti Muhimu Kati ya Mungu Mwenye Mwili na Watu Wanaotumiwa na Mungu

Kwa miaka mingi Roho wa Mungu amekuwa akitafuta bila kikomo Akifanya kazi duniani. Kwa enzi nyingi Mungu Ametumia wanadamu wengi kufanya kazi Yake. Hata hivyo Roho wa Mungu bado hana mahali pazuri pa kupumzika. Kwa hivyo Mungu hufanya kazi Yake, akisonga bila kikomo katika watu tofauti, na kwa ujumla Yeye hutumia watu ili kufanya hili. Yaani, katika miaka hii yote mingi, kazi ya Mungu haijawahi kusimama, lakini inaendelezwa mbele katika mwanadamu, mpaka siku ya leo. Ingawa Mungu Amesema na Ametenda mengi, mwanadamu bado hamjui Mungu, hii ni kwa sababu Mungu hajawahi kuonekana kwa mwanadamu na pia kwa sababu Hana umbo lililo wazi. Na hivyo Mungu lazima Akamilishe kazi hii— kuwasababisha wanadamu wote wajue umuhimu wa Mungu wa matendo. Kufikia lengo hili,

Mungu lazima afichulie wanadamu Roho Wake kwa uwazi na kufanya kazi miongoni mwao. Yaani, ni wakati tu ambapo Roho wa Mungu anaingia katika hali ya kimwili, anavaa nyama na mifupa na kutembea akionekana kati ya wanadamu, akiandamana nao katika maisha yao, wakati mwingine akionekana na wakati mwingine kujificha, ndipo wanadamu wataweza kumuelewa kwa undani zaidi. Kama Mungu daima Angebaki katika mwili, Hangeweza kumaliza kwa ukamilifu kazi Yake. Baada ya kufanya kazi katika mwili kwa kipindi cha muda, kumaliza huduma ambayo inastahili kufanyika Akiwa katika mwili, Mungu ataondoka kwenye mwili na Afanye kazi katika ulimwengu wa kiroho kwa mfano wa mwili kama vile Yesu Alivyofanya baada ya kufanya kazi kwa kipindi cha muda katika ubinadamu wa kawaida na kukamilisha kazi yote ambayo Yeye Alihitajika kukamilisha. Mnaweza kukumbuka fungu hili kutoka kwa “Njia...(5)”: “Nakumbuka Baba yangu Akiniambia, ‘Duniani, tafuta tu kufanya mapenzi ya Baba Yako na ukamilishe agizo Lake. Hakuna jambo lingine linalokuhusu Wewe.’” Je, unaona nini katika kifungu hiki? Wakati Mungu Anakuja duniani, Yeye Anafanya tu kazi Yake ndani ya uungu. Hili ndilo Roho wa mbinguni amemwaminia Mungu mwenye mwili. Anapokuja, anakwenda tu kuzungumza kila mahali, kutamka matamshi Yake kwa njia tofauti na kutoka kwa mitazamo tofauti. Yeye kimsingi Anachukulia kumruzuku mwanadamu na kumfundisha mwanadamu kama malengo Yake na kanuni Zake za kazi na hajihusishi na vitu kama uhusiano kati ya wanadamu au maelezo ya maisha ya wanadamu. Huduma Yake kuu ni kuzungumza kwa niaba ya Roho. Wakati Roho wa Mungu Anaonekana katika mwili kwa hali iliyo wazi, Yeye hukimu uzima wa mwanadamu na kuuweka wazi ukweli tu. Yeye hajihusishi katika kazi ya mwanadamu, yaani, Yeye hashiriki katika kazi ya binadamu. Binadamu hawezi kufanya kazi ya uungu, na Mungu hashiriki katika kazi za binadamu. Katika miaka yote tangu Mungu aje duniani kufanya kazi Yake, Yeye daima Ametumia wanadamu kuifanya. Lakini wanadamu hawa hawawezi kuchukuliwa kama Mungu mwenye mwili; wao wanaweza tu kuchukuliwa kama wanadamu wanaotumiwa na Mungu. Lakini Mungu wa leo Anaweza kuzungumza moja kwa moja kutoka katika mtazamo wa uungu, Akitoa nje sauti ya Roho, na kufanya kazi kwa niaba ya Roho. Wanadamu wote ambao Mungu Ametumia katika enzi zote vivyo hivyo ni mifano ya Roho wa Mungu Akifanya kazi ndani ya mwili wa nyama, hivyo basi kwa nini hawawezi kuitwa Mungu? Lakini Mungu wa leo pia ni Roho wa Mungu Anayefanya kazi moja kwa moja katika mwili, na Yesu pia Alikuwa Roho wa Mungu Aliyefanya kazi katika mwili; Wote hawa wawili wanaitwa Mungu. Basi tofauti ni gani? Katika enzi zote, wanadamu ambao Mungu Ametumia wote wana uwezo wa mawazo na mantiki ya kawaida. Wao wote wanajua kanuni za mienendo ya binadamu. Wamekuwa na mawazo ya kawaida ya binadamu, na wamemilikiwa na vitu vyote ambavyo watu wa kawaida wanapaswa kumiliki. Wengi wao wamekuwa na vipaji vya pekee na werevu wa kiasili. Katika kuwafinyanga watu hawa, Roho wa Mungu Anatumia vipaji vyao, ambavyo ni zawadi zao Alizowapa Mungu. Roho wa Mungu Anayeleta vipaji vyao katika kazi,

Akitumia uwezo wao kumhudumia Mungu. Hata hivyo, kiini cha Mungu hakina itikadi na hakina fikira. Hakiungani na mawazo ya binadamu na hata kinakosa vitu ambavyo binadamu wa kawaida huwa navyo. Yaani, Mungu hata hafahamu vizuri kanuni za maadili ya binadamu. Hivi ndivyo ilivyo Mungu wa leo Anapokuja duniani. Kazi Yake na maneno Yake hayajachafuliwa na nia au fikira za binadamu, bali ni dhihirisho la moja kwa moja la nia za Roho, na Anafanya kazi moja kwa moja kwa niaba ya Mungu. Hii ina maana kuwa Roho hunena moja kwa moja, yaani, uungu hufanya kazi moja kwa moja, bila kuchanganya ndani hata nia kidogo za mwanadamu. Yaani, Mungu katika mwili Anajumuisha uungu moja kwa moja, Hana mawazo ya binadamu au itikadi, na Haelewi kanuni za maadili ya binadamu. Kama kungekuwa na kazi ya uungu tu (kumaanisha iwapo ingekuwa Mungu mwenyewe pekee ndiye Anayefanya kazi hiyo), kazi ya Mungu haingeweza kufanyika duniani. Kwa hivyo Mungu Anapokuja duniani, lazima Awe na wanadamu wachache Anaowatumia kufanya kazi katika ubinadamu pamoja na kazi ambayo Mungu hufanya katika uungu. Kwa maneno mengine, Yeye Anatumia kazi ya mwanadamu ili kusaidia kazi Yake takatifu. La sivyo, mwanadamu hangeweza kuja katika mawasiliano ya moja kwa moja na kazi ya uungu. Hivi ndivyo ilivyokuwa baina ya Yesu na wanafunzi wake. Wakati wa maisha Yake duniani Yesu alipiga marufuku sheria za zamani na kuanzisha amri mpya. Pia alizungumza maneno mengi. Yote haya yalifanyika katika uungu. Wale wengine, kama vile Petro, Paulo, na Yohana, wote waliweka kazi yao ya baadaye juu ya msingi wa maneno ya Yesu. Yaani, Mungu alikuwa akizindua kazi Yake katika enzi hiyo, Akikaribisha mwanzo wa Enzi ya Neema; yaani, Alileta enzi mpya, Akaiondoa ile ya zamani, na pia kutimiza maneno “Mungu ni Mwanzo na Mwisho”. Kwa maneno mengine, mwanadamu lazima afanye kazi ya mwanadamu juu ya msingi wa kazi ya Mungu. Yesu alipomaliza kusema yote Aliyohitajika kusema na kumaliza kazi Yake hapa duniani, alitoka katika mwanadamu. Baada ya haya, watu wote, wakifanya kazi, walifanya hivyo kwa mujibu wa kanuni zilizoonyeshwa katika maneno Yake na kutenda kwa mujibu wa ukweli Alioongea. Hawa wote walikuwa watu waliomfanyia Yesu kazi. Kama ingekuwa ni Yesu pekee Yake akifanya kazi, haijalishi kiasi gani Yeye Angezungumza, bado wanadamu hawangeweza kuwa na uhusiano na neno Lake, kwa sababu Yeye Alifanya kazi katika uungu na angeweza tu kuzungumza maneno ya uungu, na Hangeweza kueleza mambo hadi kiwango ambacho watu wa kawaida wangeweza kuelewa maneno Yake. Hivyo basi ilimpasa kuwa na mitume na manabii waliokuja kabla Yake kuongezea kazi Yake. Hii ni kanuni ya jinsi Mungu mwenye mwili Hufanya kazi—kwa kutumia mwili wa nyama kusema na kutenda ili kukamilisha kazi ya uungu, na kisha kwa kutumia wanadamu wachache au zaidi wanaopendeza moyo wa Mungu ili kuongezea kazi Yake. Yaani, Mungu Anatumia wanadamu wanaopendeza moyo Wake kuongoza na kunyunyiza binadamu ili watu wateule wa Mungu waweze kuingia katika uhalisi wa ukweli.

Kama, katika kupata mwili, Mungu anafanya kazi ya uungu tu bila kuwa na wanadamu wachache wa ziada wanaopendeza moyo Wake kushirikiana na Yeye, basi mwanadamu hangekuwa na uwezo kabisa wa kuelewa mapenzi ya Mungu au kuwasiliana na Mungu. Mungu lazima atumie wanadamu wa kawaida wanaopendeza moyo Wake ili kukamilisha kazi hii, kutunza na kuchunga makanisa, ili kufikia kiwango ambapo mchakato wa ufahamu wa mwanadamu, ubongo wake unaweza kubuni. Kwa maneno mengine, Mungu anatumia wanadamu wachache wanaopendeza moyo wake “kutafsiri” kazi anayofanya katika uungu Wake, ili iweze kufunuliwa, yaani, kubadilisha lugha ya Mungu kuwa lugha ya binadamu, hivyo kwamba wanadamu wote waweze kuielewa, wote waifahamu. Kama Mungu hangefanya hivyo, hakuna mwanadamu angeweza kuelewa lugha takatifu ya Mungu, kwa sababu idadi ya wanadamu wanaoupendeza moyo wa Mungu, ni chache mno, na uwezo wa mwanadamu kufahamu ni dhaifu. Hiyo ndiyo maana Mungu hutumia njia hii wakati wa kufanya kazi katika mwili wa nyama. Kama kungekuwa na kazi ya uungu peke yake, mwanadamu hangeweza kabisa kujua au kuwasiliana na Mungu, kwa sababu mwanadamu haelewi lugha ya Mungu. Mwanadamu anaweza kuelewa lugha hii tu kupitia tu kwa nguvu ya wanadamu wanaopendeza moyo wa Mungu kufafanua maneno Yake. Hata hivyo, kama kungekuwa na wanadamu kama hao pekee wakifanya kazi katika ubinadamu, hilo lingeweza tu kudumisha maisha ya kawaida ya mwanadamu; lisingeweza kubadilisha tabia ya mwanadamu. Kazi ya Mungu basi haingekuwa na mwanzo mpya; kungekuwa tu na nyimbo zile zile za zamani, maelezo yale yale ya kawaida ya zamani. Ni kupitia kwa nguvu ya Mungu mwenye mwili pekee, Anayesema yote yanayohitajika kusemwa na kufanya yote ambayo yanafaa kufanywa katika kipindi cha Yeye kupata mwili, ambapo baadaye watu hufanya kazi na kupata uzoefu kulingana na maneno Yake, ndipo tabia ya maisha yao itaweza kubadilika na waweze kusonga na nyakati. Yeye ambaye Anafanya kazi katika uungu Anawakilisha Mungu, ilhali wale wanaofanya kazi katika ubinadamu ni wanadamu wanaotumiwa na Mungu. Yaani, Mungu mwenye mwili ana tofauti kubwa na wanadamu wanaotumiwa na Mungu. Mungu mwenye mwili Anaweza kufanya kazi ya uungu, lakini wanadamu wanaotumiwa na Mungu hawawezi. Mwanzoni mwa kila enzi, Roho wa Mungu huongea binafsi kuzindua enzi mpya na kuleta mwanadamu kwenye mwanzo mpya. Wakati Yeye Amemaliza kuongea, hili linaashiria kwamba kazi ya Mungu katika uungu Wake imekamiliwa. Baada ya hapo, wanadamu wote hufuata mwongozo wa wale ambao wametumiwa na Mungu kuingia katika uzoefu wa maisha. Vile vile, hii pia ni enzi ambapo Mungu huleta mwanadamu katika enzi mpya na Anampa kila mwanadamu mwanzo mpya. Kwa hilo, kazi ya Mungu katika mwili inahitimishwa.

Mungu haji duniani kufanya ubinadamu Wake wa kawaida uwe mkamilifu. Yeye haji kufanya kazi ya ubinadamu wa kawaida, ila kufanya kazi ya uungu katika ubinadamu wa

kawaida. Kile ambacho Mungu huongea kama ubinadamu wa kawaida si kile ambacho mwanadamu anakifikiria kuwa. Mwanadamu hufafanua “ubinadamu wa kawaida” kama kuwa na mke, au mume, na watoto. Huu ni ushahidi kwamba mtu ni mwanadamu wa kawaida. Lakini Mungu haoni hivi. Anaona ubinadamu wa kawaida kama kuwa na mawazo ya kawaida ya binadamu, maisha ya kawaida ya binadamu, na kuzaliwa kwa watu wa kawaida. Lakini kuwa Kwake kawaida hakuhusishi kuwa na mke, au mume na watoto vile ambavyo mwanadamu anavyozungumzia hali ya kawaida. Yaani, kwa mwanadamu, ubinadamu wa kawaida ambao Mungu Anazungumzia ni kile mwanadamu angeona kama kukosekana wa ubinadamu, karibu ukose kuwa na hisia na kuonekana hauna mahitaji ya kimwili, kama vile Yesu, Ambaye kwa nje tu alikuwa mwanadamu wa kawaida na alichukua sura ya mwanadamu wa kawaida, lakini katika kiini hakuwa kabisa na vitu alivyo navyo mwanadamu wa kawaida. Kutokana na hili inaweza kuonekana kwamba dutu ya Mungu mwenye mwili haihusishi ubinadamu wote wa kawaida, lakini sehemu tu ya mambo ambayo wanadamu wanapaswa kuwa nayo, ili kuendeleza utaratibu wa maisha ya kawaida ya binadamu na kuruzuku uwezo wa kawaida wa binadamu wa akili. Lakini hivi vitu havihusiani na kile ambacho mwanadamu anaona kama ubinadamu wa kawaida. Ni vitu ambavyo Mungu mwenye mwili Anapaswa kuwa navyo. Hata hivyo, kuna baadhi ya wanadamu wanaoshikilia kwamba Mungu mwenye mwili Anaweza tu kuwa na ubinadamu wa kawaida iwapo Yeye ana mke, watoto na familia. Bila mambo haya, wanasema, Yeye si mwanadamu wa kawaida. Nakuuliza hivi basi, je, Mungu Ana mke? Je, inawezekana kwa Mungu kuwa na mume? Je, Mungu Anaweza kuwa na watoto? Je, hizi sio dhana zenye kosa tu? Hata hivyo, Mungu mwenye mwili hawezi kuchomoka kutoka katika nyufa kwenye miamba au kuanguka chini kutoka mbinguni. Anaweza tu kuzaliwa kwa familia ya kawaida ya binadamu. Hiyo ndiyo maana Anao wazazi na madada. Haya ndiyo mambo ambayo ubinadamu wa kawaida wa Mungu mwenye mwili lazima Awe nayo. Hivi ndivyo Yesu alivyokuwa. Yesu Alikuwa na baba na mama, na ndugu. Haya yote yalikuwa ya kawaida. Lakini kama Angekuwa na mke na watoto, basi Wake haungekuwa ubinadamu wa kawaida ambao Mungu alitaka Mungu mwenye mwili awe nao. Kama hali ingekuwa hivyo, Yeye Hangekuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa niaba ya uungu. Ilikuwa hasa kwa sababu Hakuwa na mke au watoto lakini Alizaliwa na wanadamu wa kawaida katika familia ya kawaida ndipo yeye alikuwa na uwezo wa kufanya kazi ya uungu. Ili kufafanua hili zaidi, kile ambacho Mungu anaona kama mwanadamu wa kawaida ni mwanadamu aliyezaliwa katika familia ya kawaida. Mwanadamu kama huyo tu ndiye anayestahili kufanya kazi ya Mungu. Kama, kwa upande mwingine, mtu huyo angekuwa na mke, watoto, au mume, mwanadamu huyo basi hangekuwa na uwezo wa kufanya kazi ya uungu kwa sababu angekuwa tu na ubinadamu wa kawaida ambao binadamu wanataka lakini si ubinadamu wa kawaida ambao Mungu anataka. Kile ambacho Mungu huona kuwa na kile ambacho Mungu huelewa ni tofauti sana mara nyingi, havifanani kabisa. Katika hatua hii ya kazi ya Mungu kuna

mengi ambayo yanapingana na kutofautiana sana na fikra za wanadamu. Unaweza kusema kwamba hatua hii ya kazi ya Mungu hujumuisha uungu ukifanya kazi moja kwa moja, huku ukisaidiwa na ubinadamu. Kwa sababu Mungu anakuja duniani kufanya kazi Yake Mwenyewe badala ya kumruhusu mwanadamu aifanye, hiyo ndiyo maana Anajipa mwili wa nyama (katika mwanadamu wa kawaida asiye mkamilifu) ili kufanya kazi Yake. Anatumia mwili huu kuwapa wanadamu enzi mpya, kuwaambia wanadamu hatua inayofuata katika kazi Yake, na kuwataka watende kwa mujibu wa njia iliyoelezwa katika maneno Yake. Na hapo Mungu Anakamilisha kazi Yake katika mwili, na yuko karibu kuondoka kwa wanadamu, asiishi tena katika mwili wa ubinadamu wa kawaida, na badala yake kusonga mbali na mwanadamu ili kuendelea na sehemu nyingine ya kazi Yake. Kisha, kwa kutumia wanadamu wanaoupendeza moyo Wake, Anaendeleza kazi Yake hapa duniani miongoni mwa kundi hili la wanadamu, lakini katika ubinadamu.

Mungu mwenye mwili hawezi kukaa na mwanadamu milele kwa sababu Mungu Ana kazi zingine nyingi za kufanya. Yeye hawezi kufungwa katika mwili; lazima aondoe mwili ili kufanya kazi ambayo Anahitaji kufanya, ingawa Yeye hufanya kazi hiyo kwa mfano wa mwili. Wakati Mungu Anakuja duniani, Yeye hasubiri hadi Afikie umbo ambalo mwanadamu wa kawaida anapaswa kufika kabla ya kufa na kuwaacha wanadamu. Haijalishi mwili Wake ni mzee vipi, wakati kazi Yake imemalizika, Anaondoka na kumwacha mwanadamu. Hakuna kitu kama umri Kwake, Yeye hahesabu siku zake kulingana na maisha ya mwanadamu; badala yake Yeye hukamilisha maisha Yake katika mwili kulingana na hatua katika kazi Yake. Baadhi ya watu wanaweza kuhisi kwamba Mungu, kwa kuingia katika mwili, lazima akue mpaka afikie hatua fulani, Awe mwanadamu mzima, kufikia umri wa uzee, na kuondoka tu wakati mwili umeshindwa. Haya ni mawazo ya mwanadamu; Mungu hafanyi kazi kwa namna hiyo. Yeye Anakuja katika mwili kufanya kazi Anayostahili kufanya tu, bali si kuishi maisha ya kawaida ya mwanadamu ya kawaida ya kuzaliwa kwa wazazi, kuwa mtu mzima, kutengeneza familia na kuanza kazi, na kulea watoto, au kupitia panda shuka za maisha—shughuli zote za mtu wa kawaida. Mungu anapokuja duniani, huyu ni Roho wa Mungu akivaa mwili, akiingia katika mwili, lakini Mungu Haishi maisha ya mtu wa kawaida. Yeye huja tu kukamilisha sehemu moja katika mpango Wake wa usimamizi. Baada ya hapo Atawaacha wanadamu. Anapoingia katika mwili, Roho wa Mungu hakamilishi ubinadamu wa kawaida wa mwili. Badala Yake, kwa wakati ulioamuliwa kabla na Mungu, uungu unafanya kazi moja kwa moja. Kisha, baada ya kufanya yote ambayo Yeye anahitajika kufanya na kukamilisha huduma Yake kikamilifu, kazi ya Roho wa Mungu katika hatua hii imekamilika, na wakati huo maisha ya Mungu mwenye mwili yanaisha pia, bila kujali kama mwili Wake wa nyama umekamilisha maisha yake au la. Yaani, haijalishi mwili wa nyama unafika hatua gani ya maisha, muda ambao unaishi duniani, yote

hutegemea kazi ya Roho. Haihusiani na kile mwanadamu anachoona kuwa ubinadamu wa kawaida. Chukua Yesu kama mfano. Yeye Aliishi katika mwili kwa miaka thelathini na mitatu na nusu. Kuhusiana na urefu wa maisha ya mwili wa binadamu, Yeye Hakupaswa kufariki Akiwa na umri huo na Hakupaswa kuondoka. Lakini Roho wa Mungu hakujali kuhusu hayo hata kidogo. Baada ya kazi Yake kumalizika, hapo mwili ulichukuliwa, ukitoweka pamoja na Roho. Hii ni kanuni ambayo Mungu hutumia kufanya kazi katika mwili. Na hivyo, kusema kwa uzito kabisa, ubinadamu wa Mungu mwenye mwili si lenye umuhimu wa kimsingi. Kusema tena, Yeye haji duniani kuishi maisha ya mtu wa kawaida. Yeye kwanza haasisi maisha ya kawaida ya binadamu na kisha Aanze kufanya kazi. Badala Yake, alimradi tu Amezaliwa katika familia ya kawaida ya binadamu, Yeye ana uwezo wa kufanya kazi ya Mungu, ambayo haijatiwa doa na nia zap mwanadamu, ambayo si ya mwili ambayo hakika haitumii njia za jamii au kuhusisha mawazo au fikra za mwanadamu, na aidha, isiyohusiana na falsafa za binadamu za kuishi. Hii ni kazi ambayo Mungu mwenye mwili ananua kufanya, na pia ni umuhimu wa vitendo wa kupata mwili Kwake. Mungu anakuja katika mwili kimsingi kufanya hatua ya kazi inayohitaji kufanyika katika mwili, bila kupitia michakato mingine isiyo na maana, na, hana uzoefu wa mwanadamu wa kawaida. Kazi ambayo Mungu mwenye mwili anahitaji kufanya haihusishi uzoefu wa kawaida wa binadamu. Hivyo, Mungu Anakuja katika mwili ili kumaliza kazi Anayohitaji kukamilisha katika mwili. Yaliyobaki Hayamhusu. Hapitii michakato mingi isiyo ya maana hivyo. Mara kazi Yake inapokamilika, umuhimu wa kupata mwili Kwake pia unaisha. Kumaliza hatua hii kuna maana kwamba kazi ambayo Yeye Anahitajika kufanya katika mwili imekamilika, na huduma ya mwili Wake imekamilika. Lakini Yeye hawezi kuendelea kufanya kazi katika mwili kwa muda usio na mwisho. Yeye lazima aende mahali pengine kufanya kazi, mahali ambapo ni nje ya mwili. Ni kwa njia hii tu ndio kazi Yake inaweza kuwa kamili zaidi, na kupanuka vizuri zaidi. Mungu hufanya kazi kulingana na mpango Wake wa awali. Yeye Anajua vyema kazi Anayohitaji kufanya na kazi Aliyomaliza kama kiganja cha mkono Wake. Mungu humwongoza kila mwanadamu kutembelea njia ambayo Yeye tayari Ameamua. Hakuna anayeweza kuepuka hili. Ni wale tu ambao hufuata uongozi wa Roho wa Mungu ndio watakaokuwa na uwezo wa kuingia katika pumziko. Huenda ikawa kwamba, katika kazi ya baadaye, sio Mungu Atakayezungumza katika mwili ili kumwongoza mwanadamu, ila Roho anayegusika akiongoza maisha ya mwanadamu. Hapo tu ndipo mwanadamu atakuwa na uwezo thabiti wa kumgusa Mungu, kumwona Mungu, na kwa kikamilifu zaidi kuingia katika uhalisi ambao Mungu anataka, ili aweze kukamilishwa na Mungu wa vitendo. Hii ndiyo kazi ambayo Mungu ananua kukamilisha, ambayo amepanga tangu zamani. Kutokana na hili, nyote mnapaswa kuona njia ambayo mnafaa kuchukua!

Epuka Ushawishi wa Giza na Utapatwa na Mungu

Je, ushawishi wa giza ni nini? “Ushawishi wa giza” ni ushawishi wa Shetani kuwadanganya, kuwapotosha kuwafunga na kuwatawala watu; ushawishi wa shetani ni ushawishi ambao una hali ya kifo. Wale wote ambao wanaishi chini ya miliki ya shetani wamehukumiwa kuangamia.

Unawezaje kuepuka ushawishi wa giza baada ya kupata imani katika Mungu? Baada ya kumwomba Mungu kwa dhati, unaelekeza moyo wako Kwake kikamilifu. Katika hatua hii, moyo wako unasongezwa na Roho wa Mungu, uko tayari kujitoa mwenyewe kikamilifu, na katika wakati huu, umeepuka ushawishi wa giza. Kama yote ambayo mtu anafanya yanampendeza Mungu na anapatana na matakwa Yake, basi yeye ni mtu ambaye anaishi ndani ya maneno ya Mungu, yeye ni mtu anayeishi chini ya utunzaji na ulinzi wa Mungu. Kama watu hawawezi kutenda maneno ya Mungu, daima wakimpumbaza na kutenda katika namna ya uzembe na Yeye, na hawaamini katika uwepo Wake, watu kama hao wote wanaishi chini ya ushawishi wa giza. Watu ambao hawajapokea wokovu wa Mungu wote wamemilikiwa na Shetani, yaani, hao wote wanaishi chini ya ushawishi wa giza. Wale ambao hawamwamini Mungu wamemilikiwa na Shetani. Hata wale ambao wanaamini katika kuwepo kwa Mungu huenda si lazima wawe wanaishi katika nuru ya Mungu, kwa sababu wale ambao wanamwamini huenda si lazima wawe wanaishi ndani ya maneno ya Mungu, na huenda si lazima wawe watu ambao wanaweza kumtii Mungu. Mtu anamwamini tu Mungu, na kwa sababu ya kushindwa kwake kumjua Mungu, bado anaishi ndani ya sheria za zamani, anaishi ndani ya maneno yaliyokufa, anaishi katika maisha ambayo ni giza na si ya hakika, hajatakaswa kikamilifu na Mungu au kupatwa kikamilifu na Mungu. Kwa hivyo, ni dhahiri ya kwamba wale wasiomwamini Mungu wanaishi chini ya ushawishi wa giza, hata wale ambao wanamwamini Mungu huenda wakawa bado wanaishi chini ya ushawishi wake, kwa ajili Roho Mtakatifu hajatekeleza kazi juu yao. Wale ambao hawajapokea neema ya Mungu au rehema ya Mungu, na wale ambao hawawezi kuona kazi ya Roho Mtakatifu, wote wanaishi chini ya ushawishi wa giza; wale ambao wanafurahia tu neema ya Mungu na bado hawamjui pia wanaishi chini ya ushawishi wa giza wakati mwingi. Kama mtu anamwamini Mungu na bado anatumia wakati mwingi wa maisha yake akiishi chini ya ushawishi wa giza, basi kuwepo kwa mtu huyu kumepoteza maana yake, bila kutaja wale ambao hawaamini katika uwepo wa Mungu.

Wale wote ambao hawawezi kukubali kazi ya Mungu au wanaokubali kazi ya Mungu lakini hawawezi kukidhi matakwa Yake wanaishi chini ya ushawishi wa giza; wale tu wanaofuatilia ukweli na wana uwezo wa kukidhi matakwa ya Mungu watapokea baraka kutoka Kwake, na ni wao tu wataepuka ushawishi wa giza. Watu ambao hawajafunguliwa, ambao siku zote wamedhibitiwa na mambo fulani na ambao hawawezi kutoa mioyo yao kwa Mungu, ni watu ambao wako chini ya utumwa wa Shetani, na wanaoishi chini ya hali ya kifo. Wale wasio

waaminifu kwa wajibu wao wenyewe, wasio waaminifu kwa agizo la Mungu na wale ambao hawatekelezi jukumu lao kanisani wanaishi chini ya ushawishi wa giza. Wale ambao husumbua maisha ya kanisa kimakusudi, wale ambao huharibu mahusiano kati ya akina ndugu na kimakusudi, au kuweka pamoja magenge yao wenyewe, wanaishi hata zaidi chini ya ushawishi wa giza; wao wanaishi ndani ya utumwa wa Shetani. Wale walio na uhusiano usio sahihi na Mungu, walio na tamaa za kifahari daima, ambao daima wanataka kupata faida, na ambao kamwe hawatafuti mabadiliko katika tabia yao ni watu ambao wanaishi chini ya ushawishi wa giza. Wale ambao hawako imara daima, ambao hawajatilia maanani utendaji wao wa ukweli, na ambao hawatafuti kukidhi matakwa ya Mungu ila kuridhisha tu miili yao wenyewe ni watu ambao pia wanaishi chini ya ushawishi wa giza na kufunikwa katika kifo. Wale ambao hujihusisha na hila na udanganyifu wakati wa kutekeleza kazi ya Mungu, ambao wanashughulikia Mungu katika njia ya kizembe, wanamdanganya Mungu, na ambao daima hujifikiria, ni watu wanaoishi chini ya ushawishi wa giza. Wale wote ambao hawawezi kumpenda Mungu kwa dhati, ambao hawafuatilii ukweli, na wasiozingatia kubadilisha tabia yao, wanaishi chini ya ushawishi wa giza.

Kama unataka kusifiwa na Mungu, lazima kwanza uepuke ushawishi wa giza wa Shetani, ufungue moyo wako kwa Mungu, na uuelekeze kwa Mungu kikamilifu. Je, mambo ambayo unafanya kwa sasa yanasifiwa na Mungu? Umeelekeza moyo wako kwa Mungu? Je, mambo ambayo umeyafanya ni yale ambayo Mungu ametaka kutoka kwako? Je, yanaingiana na ukweli? Lazima ujichunguze kila wakati, uzingatie kula na kunywa maneno ya Mungu, uweke moyo wako wazi mbele Yake, umpende kwa uwazi, na ujitumie kwa bidii kwa ajili ya Mungu. Watu kama hao hakika watapokea sifa ya Mungu.

Wote ambao humwamini Mungu ilhali hawafuatilii ukweli hawana namna ya kuepuka ushawishi wa shetani. Wale wote ambao hawaishi maisha yao kwa uaminifu, wanaotenda kwa njia moja mbele ya wengine na njia nyingine kwa siri, wanaotoa mwonekano wa unyenyekevu, uvumilivu, na upendo ilhali katika kiini ni wenye kudhuru kwa siri, wana hila, na hawana uaminifu kwa Mungu—watu hawa ni mfano halisi wa wale wanaoishi chini ya ushawishi wa giza. Wao ni wa kizazi cha nyoka. Wale ambao imani yao katika Mungu daima ni kwa ajili ya faida zao wenyewe, ambao ni wa kujidai na wenye maringo, ambao hujigamba, na hulinda hadhi zao wenyewe ni wale wanaompenda Shetani na kuupinga ukweli. Wao wanapinga Mungu na ni wa Shetani kikamilifu. Wale ambao hawako makini kwa mizigo ya Mungu, ambao hawamtumikii Mungu kwa moyo wote, ambao daima wanajali maslahi yao wenyewe na maslahi ya familia zao, ambao hawawezi kuacha kila kitu ili wajitumie kwa ajili ya Mungu, na ambao kamwe hawaishi kulingana na maneno Yake wanaishi nje ya maneno ya Mungu. Watu kama hawa hawawezi kupokea sifa ya Mungu.

Wakati Mungu aliumba watu, ilikuwa ili kuwafanya wafurahie utajiri Wake na wampende kwa kweli; katika njia hii, watu wangeishi katika nuru Yake. Leo, wote ambao hawawezi kumpenda Mungu, ambao hawako makini kwa mizigo Yake, ambao hawawezi kutoa mioyo yao kikamilifu kwa Mungu, ambao hawawezi kuchukua moyo wa Mungu kama wao wenyewe, ambao hawawezi kubeba mizigo ya Mungu kama yao wenyewe—nuru ya Mungu haiangazi juu ya watu wowote kama hawa, kwa hivyo, wote wanaishi chini ya ushawishi wa giza. Wako kwenye njia ambayo huenda kinyume kabisa na mapenzi ya Mungu, na yote wanayoyafanya hayana hata chembe ya ukweli. Wanazamia katika matatizo na Shetani na ni wale ambao wanaishi chini ya ushawishi wa giza. Kama unaweza daima kula na kunywa maneno ya Mungu na pia kuwa makini na mapenzi Yake na kutenda maneno Yake, basi wewe ni wa Mungu, na wewe ni mtu anayeishi ndani ya maneno ya Mungu. Je, uko tayari kuepuka kumilikiwa na Shetani na kuishi katika nuru ya Mungu? Kama unaishi ndani ya maneno ya Mungu, basi Roho Mtakatifu atakuwa na nafasi ya kutenda kazi Yake; kama unaishi chini ya ushawishi wa Shetani, basi Roho Mtakatifu hatakuwa na nafasi ya kutenda kazi yoyote. Kazi ambayo Roho Mtakatifu hutenda kwa watu, nuru ambayo Yeye huangaza kwa watu, na imani ambayo Yeye hutoa kwa watu hukaa kwa muda tu; kama hawako makini na hawampi kipaumbele, kazi iliyotendwa na Roho Mtakatifu itawapita. Kama watu wanaishi ndani ya maneno ya Mungu, basi Roho Mtakatifu atakuwa pamoja nao na kutenda kazi juu yao; kama watu hawaishi ndani ya maneno ya Mungu, basi wanaishi ndani ya utumwa wa Shetani. Watu wanaoishi katika tabia ya kiufisadi hawana uwepo wala kazi ya Roho Mtakatifu. Kama unaishi ndani ya nyanja ya maneno ya Mungu, kama unaishi katika hali inayohitajika na Mungu, basi wewe ni Wake na kazi Yake itatendwa juu yako; kama huishi ndani ya nyanja ya matakwa ya Mungu lakini badala yake unamilikiwa na Shetani, basi hakika wewe unaishi chini ya upotovu wa Shetani. Ni kwa kuishi ndani ya maneno ya Mungu tu na kutoa moyo wako Kwake, ndipo unaweza kukidhi matakwa Yake; lazima ufanye asemavyo Mungu, lazima ufanye maneno ya Mungu msingi wa kuwepo kwako na hali halisi ya maisha yako, na ni hapo tu ndipo utakuwa wa Mungu. Kama kwa dhati unatenda kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu, Atatenda kazi juu yako na kisha utaishi chini ya baraka za Mungu, uishi katika nuru ya uso wa Mungu, kufahamu kazi ambayo Roho Mtakatifu hutenda, na pia kuhisi furaha ya uwepo wa Mungu.

Kuepuka ushawishi wa giza, lazima kwanza uwe mwaminifu kwa Mungu na kuwa na hamu ya kufuatilia ukweli—ni hapo tu ndipo utakuwa na hali sahihi. Kuishi katika hali sahihi ndilo sharti la mwanzo la kuepuka ushawishi wa giza. Kukosa hali sahihi ina maana kwamba wewe si mwaminifu kwa Mungu na ya kwamba huna hamu ya kutafuta ukweli. Basi, kuepuka ushawishi wa giza hakutawezekana. Mtu kuepuka ushawishi wa giza ni kwa msingi wa maneno Yangu, na kama mtu hawezi kutenda kwa mujibu wa maneno Yangu, hataepuka utumwa wa ushawishi wa

giza. Kuishi katika hali sahihi ni kuishi chini ya uongozi wa maneno ya Mungu, kuishi katika hali ya kuwa mwaminifu kwa Mungu, kuishi katika hali ya kutafuta ukweli, kuishi katika uhalisi wa kugharamia rasilimali kwa ajili ya Mungu kwa dhati, kuishi katika hali ya kumpenda Mungu kwa kweli. Wale ambao wanaishi katika hali hizi na ndani ya hali halisi hii watabadilika hatua kwa hatua wanapoingia ndani zaidi katika ukweli, nao watabadilika kwa kuongezeka kwa kazi, mpaka hatimaye hakika watapatwa na Mungu, na watakuja kwa kweli kumpenda Mungu. Wale ambao wameepuka ushawishi wa giza wataweza kufahamu mapenzi ya Mungu hatua kwa hatua, wataelewa mapenzi ya Mungu hatua kwa hatua, na hatimaye kuwa wasiri wa Mungu. Hawatakosa dhana kumhusu Mungu tu, na kukosa uasi dhidi Yake, lakini watakuja kuchukia hata zaidi dhana na uasi ambao walikuwa nao kabla, kusababisha upendo wa kweli kwa Mungu mioyoni mwao. Wale ambao hawawezi kuepuka ushawishi wa giza wanashughulika na miili yao, na wamejaa uasi; mioyo yao imejazwa dhana za kibinadamu na falsafa za kuishi, pamoja na nia zao na majadiliano. Mungu anataka upendo mmoja wa mtu, naye humhitaji mtu amilikiwe na maneno Yake na upendo wa mtu Kwake. Kuishi ndani ya maneno ya Mungu, kugundua kile ambacho mtu anapaswa kutafuta kutoka ndani ya maneno Yake, kumpenda Mungu kama matokeo ya maneno Yake, kukimbiakimbia kwa ajili ya maneno ya Mungu, kuishi kwa ajili ya maneno ya Mungu—haya yote ni mambo ambayo mtu anapaswa kufikia. Kila kitu lazima kijengwe kulingana na maneno ya Mungu, na hapo tu ndipo mtu ataweza kukidhi matakwa ya Mungu. Kama mwanadamu hajatayarishwa na maneno ya Mungu, basi yeye ni funza tu ambaye amemilikiwa na Shetani. Yapime moyoni mwako mwenyewe—ni maneno mangapi ya Mungu ambayo umekita mizizi yake ndani yako? Ni katika mambo gani unaishi kulingana na maneno Yake? Ni katika mambo gani ndiyo hujakuwa ukiishi kulingana nayo? Kama maneno ya Mungu hayajakumiliki kikamilifu, basi ni nini hasa kilicho moyoni mwako? Katika maisha yako ya kila siku, je, unadhibitiwa na Shetani, au unamilikiwa na maneno ya Mungu? Je, maombi yako yameanzishwa kutoka kwa maneno Yake? Je, umeondoka katika hali yako mbaya kupitia nuru ya maneno ya Mungu? Kuchukua maneno ya Mungu kama msingi wa kuwepo kwako, hili ndio jambo kila mtu anapaswa kuingia ndani. Kama maneno ya Mungu hayapo katika maisha yako, basi unaishi chini ya ushawishi wa giza, wewe ni muasi dhidi ya Mungu, unampinga Mungu, na huheshimu jina Lake—imani ya watu kama hao katika Mungu ni uharibifu na usumbufu kabisa. Je, ni kiasi gani cha maisha yako kimeishiwa kwa mujibu wa maneno Yake? Ni kiasi gani cha maisha yako hakijaishiwa kwa mujibu wa maneno Yake? Je, ni kiasi gani cha kile ambacho maneno ya Mungu yamehitaji kwako kimetimizwa ndani yako? Ni mangapi yamepotea ndani yako? Je, umechunguza mambo kama hayo kwa karibu?

Kuepuka ushawishi wa giza, kipengele kimoja ni kwamba kunahitaji kazi ya Roho Mtakatifu, na kipengele kingine ni kwamba kunahitaji ushirikiano wa kujitolea kutoka kwa mtu.

Mbona Nasema ya kwamba mtu hayuko kwenye njia sahihi? Kwanza, kama mtu yuko kwenye njia sahihi, ataweza kutoa moyo wake kwa Mungu, ambayo ni jukumu linalohitaji muda mrefu kuingia ndani kwa sababu mwanadamu daima amekuwa akiishi chini ya ushawishi wa giza na amekuwa chini ya utumwa wa Shetani kwa maelfu ya miaka. Kwa hivyo, kuingia huku hakuwezi kupatikana katika siku moja au mbili. Nilileta suala hili leo ili watu waweze kuwa na ufahamu wa hali yao wenyewe; kuhusu ushawishi wa giza ni nini na kuishi ndani ya nuru ni nini, kuingia kunawezekana wakati mtu ana uwezo wa kutambua mambo haya. Hii ni kwa sababu ni lazima ujue ushawishi wa Shetani ni nini kabla uuepuke, na hapo tu ndipo utakuwa na njia ya kuuepuka hatua kwa hatua mwenyewe. Kuhusu ni nini cha kufanya baada ya hapo, hilo ni suala la wanadamu wenyewe. Lazima daima uingie kutoka mtazamo mwema na hupaswi kusubiri kamwe kwa utulivu. Ni kwa njia hii tu ndiyo unaweza kupatwa na Mungu.

Katika Imani, Mtu Lazima Alenge Ukweli—Kujihusisha na Kaida za Dini Sio Imani

Je, ni desturi ngapi za kidini unazozizingatia? Ni mara ngapi umeasi dhidi ya neno la Mungu na kwenda kwa njia yako? Ni mara ngapi umetia katika vitendo neno la Mungu kwa sababu kwa kweli unajali mizigo Aliyobeba na unatafuta kutimiza mapenzi Yake? Lielewe neno la Mungu na uliweke katika vitendo. Kuwa mwenye maadili katika vitendo na matendo yako; huku si kutii sheria au kufanya hivyo shingo upande kwa ajili ya kujionyesha. Badala yake, huku ni kutenda ukweli na kuishi kulingana na neno la Mungu. Vitendo kama hivi pekee ndivyo humridhisha Mungu. Desturi yoyote inayompendeza Mungu si kanuni bali ni kutenda ukweli. Wanadamu wengine wana upendeleo wa kujivutia nadhari. Mbele ya ndugu zao, wanasema kweli ni wadeni wa Mungu, lakini akiwapa kisogo, hawatendi ukweli ila wanafanya tofauti kabisa. Je, hawa si ni Mafarisayo wa dini? Mtu ambaye anampenda Mungu kwa kweli na ana ukweli ni yule ambaye ni mwaminifu kwa Mungu, lakini bila ya hafichui kwa nje. Yeye yuko tayari kutenda ukweli wakati mambo yanapotokea wala hasemi au kutenda kinyume cha dhamiri yake. Anaonyesha hekima wakati mambo yanapotokea na ni mwenye maadili katika matendo yake, bila kujali hali. Mtu kama huyu ni mtu ambaye anahudumu kwa kweli. Kuna watu wengine ambao mara nyingi shukrani zao kwa kuwa wadeni wa Mungu ni kwa mdomo tu. Siku zao huisha wakiwa na nyuso za wasiwasi, kuonekana wameathiriwa, na kuvalia nyuso za huzuni. Hali ya kuchukiza kweli! Na kama ungewauliza, “Ni kwa njia zipi wewe ni mdeni wa Mungu? Tafadhali niambie!” Hawangeweza kutamka lolote. Kama wewe ni mwaminifu kwa Mungu, basi usizungumze kwa nje kuhusu hilo; badala yake, onyesha upendo wako kwa Mungu kwa njia ya matendo halisi, na kumwomba kwa moyo wa kweli. Wale wanaotumia maneno pekee kushughulika na Mungu ni wanafiki wote! Baadhi yao husema kuwa wao ni wadeni kwa Mungu

katika kila sala, na kuanza kulia wakati wowote wanaposali, hata bila kuguswa na Roho Mtakatifu. Watu kama hawa wamepagawa na kaidi na fikira za kidini; wanaishi kulingana na hizo kaidi na fikra, daima wakiamini kwamba matendo kama hayo humpendeza Mungu, na kwamba kumcha Mungu kijuujuu au machozi ya huzuni ndivyo Mungu hupendelea. Ni kitu kipi kizuri kinachoweza kutoka kwa watu kama hao wa kushangaza? Ili kuonyesha unyenyekevu wao, baadhi yao huonyesha neema bandia wakati wanapozungumza mbele ya watu wengine. Baadhi yao kwa makusudi ni wanyonge mbele ya watu wengine, kama mwanakondoo asiye na nguvu yoyote. Je, hii ni tabia ya watu wa ufalme? Mtu wa ufalme sharti awe wa kusisimua na aliye huru, asiye na hatia na aliye na uwazi, mwaminifu na wa kupendeza; mtu aishiye katika hali ya uhuru. Ana uadilifu na heshima, na anaweza kushuhudia kokote aendako; yeye ni yule anayependwa na Mungu na wanadamu. Wale ambao ni wanafunzi katika imani huwa na matendo mengi ya nje; lazima kwanza wapitie kipindi cha ushughulikiaji na kuvunjwa. Wale ambao wana imani kwa Mungu katika nyoyo zao hawawezi kutofautishwa na wengine kwa nje, lakini vitendo na matendo yao ni ya kupongezwa kwa wengine. Watu wa aina hii pekee ndio wanaoweza chukuliwa kuwa wanaishi kwa kudhihirisha neno la Mungu. Ukihubiri injili kila siku kwa mtu huyu na yule, ukiwaleta kwa wokovu, ilhali mwishowe, wewe bado unaishi katika sheria na mafundisho, basi wewe huwezi kuleta utukufu kwa Mungu. Watu wa aina hii ni watu wa dini, na wanafiki pia.

Kila mara watu wa kidini kama hao wanapokusanyika, wanauliza, “Dada, umeshinda vipi siku hizi?” Anajibu, “Nahisi kuwa mimi ni mdeni wa Mungu na siwezi kuridhisha matakwa ya moyo Wake.” Mwingine anasema, “Mimi, pia, ni mdeni wa Mungu na nimeshindwa kumkidhi.” Sentensi na maneno haya machache pekee yanaonyesha mambo maovu yaliyo ndani ya nyoyo zao. Maneno kama hayo ni ya kuchukiza zaidi na yenye makosa sana. Asili ya watu kama hao inampinga Mungu. Wale ambao huzingatia uhalisi huwasilisha vyovyote vilivyomo katika nyoyo zao na kufungua mioyo yao katika mawasiliano. Hakuna shughuli hata moja ya uongo, hakuna heshima ama salamu na mazungumzo matupu. Wao daima huwa na uwazi na hawafuati sheria za duniani. Kuna wale ambao wako na upendeleo wa kujionyesha kwa nje, hata bila maana yoyote. Wakati mwingine anaimba, yeye anaanza kukatika, bila hata kugundua kuwa wali katika sufuria yake umeshaungua. Watu wa aina hii si wacha Mungu au waheshimiwa, bali ni watu wa kijinga kupindukia. Hizi zote ni maonyesho ya ukosefu wa ukweli! Wakati watu wengine wanawasiliana kuhusu masuala ya maisha katika roho, ingawa hawasemi kuhusu kuwa wadeni wa Mungu, wao hubaki na upendo wa kweli kwa Mungu ndani ya mioyo yao. Kuwa kwako mdeni kwa Mungu hakuhusiani na watu wengine; wewe ni mdeni kwa Mungu, si kwa mwanadamu. Kwa hiyo ina maana gani wewe daima kuzungumzia haya kwa watu wengine? Lazima uweke umuhimu kwa kuingia katika uhalisi, si kwa bidii au maonyesho ya nje.

Je, matendo mazuri ya kijuujuu ya mwanadamu yanawakilisha nini? Hayo huwakilisha mwili, na hata matendo yaliyo bora zaidi ya nje hayawakilishi maisha, ila tabia yako tu mwenyewe. Matendo ya nje ya mwanadamu hayawezi kutimiza matakwa ya Mungu. Wewe daima huzungumza kuhusu udeni wako kwa Mungu, lakini huwezi kuyaruzuku maisha ya wengine au kuwafanya wengine kumpenda Mungu. Je, unaamini kwamba matendo kama hayo yatamridhisha Mungu? Unaamini kwamba hii ndiyo matakwa ya moyo wa Mungu, kwamba haya ni ya roho, lakini kwa kweli huu ni ujinga! Unaamini kwamba yale yanayokupendeza wewe na unayotaka ni yale yanayomfurahisha Mungu. Je, yanayokupendeza yanaweza kuwakilisha yanayompendeza Mungu? Je, tabia ya mwanadamu inaweza kumwakilisha Mungu? Yale yanayokupendeza wewe ndiyo hasa yale humchukiza Mungu, na mienendo yako ni ile ambayo Mungu huchukia na kukataa. Kama unahisi kuwa wewe ni mdeni, basi nenda na usali mbele za Mungu. Hakuna haja ya kuzungumzia jambo hilo kwa watu wengine. Usipooomba mbele za Mungu na badala yake mara kwa mara unajivuta nadhari kwako mbele ya wengine, jambo hili linaweza kutimiza matakwa ya moyo wa Mungu? Kama matendo yako daima yanaonekana tu, hii ina maana kuwa wewe ni mtu bure zaidi ya wote. Ni mtu wa aina gani yule aliye na matendo mazuri ya kijuujuu tu lakini hana uhalisi? Watu kama hao ni Mafarisayo wanafiki na watu wa dini! Msipoacha matendo yenu ya nje na hamuwezi kufanya mabadiliko, basi dalili za unafiki ndani yenu zitazidi kuimarika. Kadiri dalili za unafiki zinavyozidi, ndivyo upinzani kwa Mungu unavyozidi, na mwishowe, watu wa aina hii hakika watatupiliwa mbali!

Ni Wale tu Wanaojua Kazi ya Mungu Leo Ndio Wanaoweza Kumhudumia Mungu

Ili uwe na ushuhuda kwa Mungu na kuliaibisha joka jekundu ni sharti uwe na kanuni, na sharti: Katika moyo wako ni lazima umpende Mungu na uingie katika maneno ya Mungu. Kama huingii katika maneno ya Mungu, basi hutakuwa na njia ya kumuaibisha Shetani. Katika ukuaji wa maisha yako, unalikataa joka kuu jekundu na kuliletea aibu kamili, na ni hapo tu ndipo hili joka jekundu kweli linaaibika. Kadiri unavyohiari kuyaweka maneno ya Mungu katika vitendo, ndivyo unavyohibitisha kwamba unampenda Mungu na kulichukia joka kuu jekundu; kadiri unavyotii maneno ya Mungu, ndivyo unavyohibitisha kwamba unautamani ukweli. Watu ambao hawayatamani maneno ya Mungu ni watu wasio na uzima. Watu kama hao ni wale walio nje ya maneno ya Mungu, walio ndani ya dini. Wanaomwamini kweli Mungu huwa na ufahamu wa kina wa maneno ya Mungu kupitia kula na kunywa maneno ya Mungu. Ikiwa huyatamani maneno ya Mungu, basi huwezi kweli kula na kunywa haya maneno ya Mungu, na kama huna ufahamu wa maneno ya Mungu, basi huna njia ya kumshuhudia Mungu au kumtosheleza Mungu.

Katika imani yako kwa Mungu, utamjuaje Mungu? Unapaswa kumjua Mungu kupitia maneno na kazi ya leo ya Mungu, bila upotovu au uwongo, na hata kabla jambo lolote lile ni sharti uijue kazi ya Mungu. Huu ndio msingi wa kumjua Mungu. Huo uwongo wa aina mbalimbali unaokosa ukubalifu wa maneno ya Mungu ni dhana za kidini, ni ukubalifu ambao ni potovu na wenye makosa. Ujuzi mkubwa zaidi wa watu mashuhuri wa kidini ni kuyachukua maneno ya Mungu yaliyokuwa yakikubalika zamani na kuyalinganisha na maneno ya Mungu ya leo. Unapomhudumia Mungu wa leo, ikiwa unashikilia vitu vilivyoangaziwa nuru na Roho Mtakatifu hapo zamani, basi huduma yako itasababisha hitilafu na vitendo vyako vitakuwa vimepitwa na wakati na havitakuwa tofauti na ibada ya kidini. Ikiwa unaamini kuwa wanaomhudumia Mungu wanafaa kuwa wanyenyekevu na wavumilivu..., na ukiweka ufahamu wa aina hii katika vitendo leo hii, basi vitendo kama hivi ni dhana ya kidini, na vitendo kama hivyo ni maigizo ya kinafiki. “Dhana za kidini” inarejelea vitu vilivyopitwa na wakati (kutia ndani ukubalifu wa maneno yaliyonenwa na Mungu zamani na kufichuliwa na Roho Mtakatifu), na vikiwekwa katika vitendo leo, basi vitahitilafiana na kazi ya Mungu na havitamfaidi mwanadamu. Iwapo mwanadamu hawezi kuyatakasa dhana za kidini yaliyomo ndani yake, basi yatakuwa kizuizi kizito katika kumuhudumia Mungu. Walio na dhana za kidini hawana njia ya kuendelea sawia na hatua za kazi ya Roho Mtakatifu, watakuwa nyuma hatua moja, halafu mbili—kwani hizi dhana za kidini humfanya mwanadamu kuwa mtu wa kujitukuza na mwenye kiburi. Mungu hahisi kumbukumbu kwa ajili ya Alichokinena na kukifanya hapo zamani; kama kimepitwa na wakati, basi Anakiondoa. Hakika unaweza kuziacha dhana zako? Ukiyakatalia maneno aliyoyanena Mungu hapo zamani, je hili linadhihirisha kuwa unaijua kazi ya Mungu? Kama huwezi kukubali mwangaza wa Roho Mtakatifu leo na badala yake unashikilia mwangaza wa zamani, hili laweza kuthibitisha kuwa unafuata nyayo za Mungu? Je, bado huwezi kuziacha dhana za kidini? Ikiwa ndivyo ilivyo, basi utakuwa mpinga Mungu.

Mwanadamu akiacha dhana za kidini, basi hatatumia akili yake kuyapima maneno na kazi ya Mungu leo hii, na badala yake atatii moja kwa moja. Japokuwa kazi ya Mungu ya leo inaonekana wazi tofauti na ya zamani, unaweza kuiacha mitazamo ya zamani na kutii moja kwa moja kazi ya Mungu leo hii. Kama unaweza kuwa na ufahamu kama huu kwamba unaonea fahari nafasi ya kazi ya Mungu leo bila kujali Alivyofanya kazi zamani, basi wewe ni mtu aliyeyaacha dhana zake, anayemtii Mungu na anayeweza kuitii kazi na maneno ya Mungu na kufuata nyayo za Mungu. Katika hili, kwa hakika, utakuwa mtu anayemtii Mungu. Huichambui au kuitafiti kazi ya Mungu; ni kana kwamba Mungu amesahau kazi Yake ya zamani, nawe pia ukaisahau. Sasa ni sasa, na zamani ni zamani, na kwa sababu leo Mungu ameyaweka kando Aliyoyafanya zamani, haifai uendelee kuyashikilia. Hapo ndipo utakuwa mtu anayemtii kabisa anayemsikia Mungu na aliyeacha kabisa dhana zake za kidini.

Kwa sababu kazi ya Mungu mara zote huwa na masuala mapya, kuna kazi ambayo inakuwa iliyopitwa na wakati na nzee kazi mpya inapoibuka. Hizi aina tofauti tofauti za kazi, nzee na mpya, hazikiniani, bali zinatoshlezana, kila hatua ikifuata iliyotangulia. Kwa kuwa kuna kazi mpya, mambo ya zamani, kwa hakika, ni sharti yaondolewe. Kwa mfano, baadhi ya vitendo vilivyokita mizizi na misemo ya mwanadamu iliyozoeleka, kuongeza juu miaka mingi ya mazoea na mafundisho ya mwanadamu, ilimuumbia mwanadamu kila aina ya dhana. Maelezo ya mwanadamu kuhusu dhana kama hizi ni kwamba bado Mungu hajafichua uso Wake halisi na tabia Yake asili kwa mwanadamu, pamoja na kuenea kwa nadharia za kale kwa miaka mingi yamekuwa ya kupendelea uundaji wa mwanadamu wa fikira kama hizo. Inaweza kusewa kwamba, katika kipindi cha imani ya mwanadamu kwa Mungu, ushawishi wa fikira mbalimbali umesababisha kutengenezwa na kubadilika kwa ufahamu wote wa fikira kumhusu Mungu ndani ya watu, jambo ambalo limewafanya watu wengi wa kidini wanaomtumikia Mungu wageuke kuwa adui Zake. Hivyo, kadiri fikira za watu za kidini zinavyokuwa thabiti, ndivyo wanavyozidi kumpinga Mungu, na ndivyo wanavyozidi kuwa maadui wa Mungu. Kazi ya Mungu daima huwa mpya, si kongwe na huwa haitengenezi mafundisho ya kidini na badala yake inabadilika kila mara na kuwa mpya kwa kiwango fulani. Kazi hii ni onyesho la tabia ya asili ya Mungu Mwenyewe. Vilevile ni kanuni ya asili ya kazi ya Mungu na mojawapo ya njia ambazo Mungu hutimiza usimamizi Wake. Iwapo Mungu asingefanya kazi kwa njia hii, mwanadamu asingebadilika au kuweza kumfahamu Mungu, na Shetani asingeshindwa. Hivyo basi, kila mara katika kazi Yake, kunatokea mabadiliko ambayo yanaonekana hayatabiriki, ila ambayo, kwa hakika, yana kipindi chake. Njia mwanadamu anavyomwamini Mungu hata hivyo ni tofauti. Anashikilia mifumo ya zamani ya kidini na kadiri yalivyo ya zamani, ndivyo yanavyokuwa ya kupendeza kwake. Akili ya kipumbavu ya mwanadamu, akili isiyobadilika kama mawe inawezaje kukubali kazi nyingi isiyoeleweka mpya na maneno ya Mungu? Mwanadamu anamchukia Mungu ambaye ni mpya kila siku na si wa zamani; anampenda tu Mungu wa zamani, ambaye ni mzee kwa umri, aliyejaa mvi na Asiyekwama papo hapo. Hivyo, kwa sababu Mungu na mwanadamu kila mmoja analo alipendalo, mwanadamu amekuwa adui wa Mungu. Kwa kiwango kikubwa, huu utata upo hata leo, wakati ambao Mungu amekuwa akifanya kazi mpya kwa takribani miaka 6000. Hawawezi kusaidika. Labda ni kwa sababu ya usumbufu wa mwanadamu, au kutokiukwa kwa kazi ya Mungu—ila hawa wahubiri bado wanashikilia vitabu vizee na karatasi ilhali Mungu anaendelea na kazi Yake ambayo haijakamilika ya usimamizi kana kwamba hana msaidizi. Japo huu utata unaleta uadui kati ya mwanadamu na Mungu, kiasi kwamba hawapatanishiki, Mungu haujali ukinzani huu. Hata hivyo mwanadamu bado anashikilia imani na dhana zake, na kamwe haiachilii. Ila kitu kimoja kiko wazi: Japo mwanadamu haachi misimamo yake, Mungu mara zote anapiga hatua na kubadilisha misimamo Yake kulingana na muktadha na hatimaye ni mwanadamu atakayeshindwa bila mapambano. Mungu ndiye adui

mkubwa zaidi wa maadui wake walioshindwa na vilevile ni bingwa wa wale miongoni mwa wanadamu ambao wameshindwa na wale ambao bado hawajashindwa. Ni nani anaweza kushindana na Mungu na ashinde? Dhana za mwanadamu zinaonekana kutoka kwa Mungu kwani wengi wao walizaliwa kipindi cha kazi ya Mungu. Na bado Mungu hamsamehei mwanadamu kwa sababu ya hili na hata zaidi Hammiminii sifa mwanadamu kwa “kumzalishia Mungu” mazao baada ya mazao ambayo yamo nje ya kazi ya Mungu. Badala yake, Yeye hughadhabishwa sana na fikira na imani za zamani za uungu, za mwanadamu na hata hachukui hatua kufikira tarehe ambayo hizi fikira zilitokea mara ya kwanza. Hakubali kamwe kwamba hizi dhana zinaletwa na kazi Yake kwani dhana za mwanadamu husambazwa na mwanadamu; chanzo chao ni fikira na akili za mwanadamu, na si Mungu, ila ni Shetani. Madhumuni ya Mungu mara zote ni kuona kazi Yake ikiwa mpya na hai, si kongwe na iliyokufa, na kile Anachotaka mwanadamu ashikilie kwa nguvu kinabadilika kulingana na enzi na kipindi, na si cha kudumu milele na kisichobadilika. Hii ni kwa sababu Yeye ni Mungu ambaye husababisha mwanadamu kuishi na kuwa mpya, tofauti na ibilisi anayemsababishia mwanadamu kufa na kuwa mzee. Je, bado hamlielewi hili? Una dhana kuhusu Mungu na umeshindwa kuziacha kwa kuwa hutafakari. Si kwa sababu kuna maana kidogo sana ndani ya kazi ya Mungu, wala kwa sababu kazi ya Mungu inatofautiana na matakwa ya binadamu, wala kwamba Mungu mara zote ni “mzembe katika wajibu Wake.” Huwezi kuacha dhana zako kwa kuwa umepungukiwa na utiifu, na huna sifa hata kidogo za kiumbe wa Mungu, na si kwamba Mungu anakufanyia mambo kuwa magumu. Yote haya umejisababishia na hayana uhusiano na Mungu; mateso na misukosuko yote husababishwa na mwanadamu. Dhamira za Mungu mara zote huwa nzuri: hakisudii kukufanya uzitoe dhana, ila angependa ubadilike na uwe mpya kadiri enzi zinavyopita. Ila bado huwezi kutofautisha chokaa na jibini na kila mara ama unachunguza au unachanganua. Si kwamba Mungu anakufanyia mambo kuwa magumu, ila ni kuwa humheshimu Mungu na uasi wako umezidi. Kiumbe mdogo anathubutu kuchukua sehemu ndogo ya kile alichopewa mwanzo na Mungu, na kisha kubadilika na kukitumia kumvamia Mungu—je, huu si uasi wa mwanadamu? Ni haki kusema kuwa binadamu hawana sifa kabisa za kutoa maoni yao mbele za Mungu, na sembuse hawana sifa za kuonyesha hadharani maneno yao yasiyo na thamani, yanukayo, yaliyooza wapendavyo—bila kutaja chochote kuhusu hizo fikira zilizooza. Haina maana?

Mtu anayemhudumia Mungu kwa ukweli ni Yule anayeita futa roho ya Mungu na anayefaa kutumiwa na Mungu na anayeweza kuacha dhana zake za kidini. Ikiwa unataka kunywa na kula kwako kwa maneno ya Mungu kuzaa matunda, basi ni sharti uache dhana zako za kidini. Ikiwa unataka kumhudumia Mungu, basi ni muhimu zaidi kuacha dhana zako za kidini na kutii maneno ya Mungu kwa kila unachokifanya. Hizi ni sifa za lazima kwa yeyote anayemhudumia Mungu.

Ukikosa ufahamu huu, punde tu unapohudumu utasababisha hitilafu na usumbufu, na ukiendelea kushikilia dhana zako, basi bila shaka utagongwa chini na Mungu, usinyanyuke daima. Chukulia wakati wa sasa kama mfano. Mengi ya matamshi na kazi za leo hazilingani na Biblia pamoja na kazi zilizofanywa na Mungu hapo awali, na kama huna nia ya kutii, basi unaweza kuanguka wakati wowote. Ikiwa unataka kuhudumu kulingana na mapenzi ya Mungu, basi unapaswa kuziacha kwanza dhana zako za kidini na urekebishe mitazamo yako. Mengi ya yale yatakayosemwa katika siku za usoni hayatalingana na yaliyosemwa zamani na ikiwa sasa unakosa nia ya kutii, hutaweza kuipita njia iliyo mbele yako. Ikiwa njia moja ya Mungu ya kufanya kazi imechipuka ndani yako na huachii dhana zako, basi njia hii itakuwa dhana zako za kidini. Ikiwa kile Mungu Alichokimekita mizizi ndani yako, basi umepata ukweli, na ikiwa maneno na ukweli wa Mungu unaweza kuwa maisha yako, kamwe hutakuwa na dhana kuhusu Mungu. Walio na ufahamu wa kweli kuhusu Mungu hawatakuwa na dhana na hawatatii mafundisho ya kidini.

Uliza maswali haya ili uwe macho:

1. Je, ufahamu ulio ndani yako unahitilafiana na huduma yako kwa Mungu?
2. Ni vitendo vingapi vya kidini vimo ndani ya maisha yako ya kila siku? Ikiwa unaonekana tu kama unamchaji Mungu, je, hili linamaanisha kuwa maisha yako yamekua na kukomaa?
3. Unapokula na kunywa maneno ya Mungu, je, unaweza kuachia dhana zako za kidini?
4. Je, una uwezo wa kutupilia mbali ibada za kidini uombapo?
5. Je, unafaa kutumiwa na Mungu?
6. Ni kiwango gani cha ufahamu wako kuhusu Mungu kina dhana za kidini?

Upendo Halisi kwa Mungu ni wa Hiari

Watu wote wamepitia usafishaji kwa sababu ya maneno ya Mungu. Kama sio Mungu mwenye mwili wanadamu bila shaka hawangebarikiwa kuteseka hivyo. Inaweza pia kusemwa hivi—wale wanaoweza kukubali majaribio ya maneno ya Mungu ni watu waliobarikiwa. Kulingana na ubora wa akili wa watu wa asili, mwenendo wao, mitazamo yao kwa Mungu, hawastahili kupokea aina hii ya usafishaji. Ni kwa sababu wameinuliwa na Mungu ndio wamefurahia baraka hii. Watu walikuwa wakisema kwamba hawakustahili kuuona uso wa Mungu au kusikia maneno Yake. Leo ni kwa sababu tu ya kutiwa moyo na Mungu na fadhili Zake ndio watu wamepokea usafishaji wa maneno Yake. Hii ni baraka ya kila mtu ambaye anazaliwa katika siku za mwisho—je, nyinyi binafsi mmepitia haya? Ni katika hali zipi watu

wanapaswa kuteseka na kuwa na vipingamizi imekusudiwa na Mungu, na haitegemei mahitaji ya watu wenyewe. Hii ni kweli kamili. Kila muumini anapaswa kuwa na uwezo wa kupitia majaribio ya maneno ya Mungu na kuteseka ndani ya maneno Yake. Je, hili ni jambo mnaloweza kuliona dhahiri? Kwa hiyo kuteseka ulikopitia kumebadilishana na baraka za leo; ikiwa hutateseka kwa ajili ya Mungu, huwezi kupata sifa Zake. Labda umelalamika hapo awali, lakini haijalishi umelalamika kiasi gani Mungu hakumbuki hayo kukuhusu wewe. Leo imekuja na hakuna haja ya kuchunguza masuala ya jana.

Watu wengine husema kwamba wao hujaribu kumpenda Mungu lakini hawawezi, na wanaposikia kwamba Mungu yuko karibu kuondoka basi wanakuwa na upendo Kwake. Watu wengine kwa jumla huwa hawaweki ukweli katika matendo, na wanaposikia kwamba Mungu yuko karibu kuondoka kwa hasira wao huja mbele Yake na kuomba. “Ee Mungu! Tafadhali usiende. Nipe nafasi! Mungu! Sijakuridhisha hapo awali; nimekuwa mdeni Wako na kukupinga Wewe. Leo niko radhi kuutoa mwili na moyo wangu kikamilifu ili hatimaye nikuridhishe na kukupenda Wewe. Sitakuwa na nafasi hiyo tena.” Umfanya aina hiyo ya ombi? Mtu anapoomba kwa njia hii ni kwa kuwa dhamiri yake imeamshwa na maneno ya Mungu. Binadamu wote ni wazito na wenye akili goigoi. Ni wenye kupatwa mara kwa mara na kuadibu na usafishaji ilhali hawajui kile ambacho Mungu anatimiza. Mungu asingefanya kazi hivi, watu bado wangechanganyikiwa; hakuna ambaye angetia msukumo hisia za kiroho ndani ya mioyo ya watu. Ni maneno ya Mungu ya hukumu na kuwafichua watu tu ndiyo yanaweza kuzaa tunda hilo. Kwa hiyo, mambo yote yanafanikishwa na kutimizwa kwa sababu ya maneno ya Mungu, na ni kwa ajili tu ya maneno Yake ndio upendo wa wanadamu kwa Mungu umeamshwa. Ikiwa watu wangempenda tu Mungu kutegemea dhamiri zao hawangeona matokeo yoyote. Watu hawakutegemeza upendo wao kwa Mungu juu ya dhamiri yao hapo awali? Kulikuwa na mtu mmoja ambaye alianza kumpenda Mungu? Ilikuwa tu kupitia kwa himizo la maneno ya Mungu ndio walimpenda Mungu. Watu wengine husema: “Nimemfuata Mungu kwa miaka mingi sana na kufurahia kiasi kikubwa cha neema Yake, baraka nyingi sana. Nimepatwa mara kwa mara na usafishaji na hukumu kutoka kwa maneno Yake. Kwa hiyo nimekuja kuelewa mengi, na nimeona upendo wa Mungu. Lazima nimshukuru Yeye, lazima nilipe neema Yake. Nitamridhisha Mungu na kifo, na nitategemeza upendo wangu Kwake juu ya dhamiri yangu.” Watu wakitegemea tu hisia za dhamiri zao, hawawezi kuhisi kupendeza kwa Mungu; wakitegemea tu dhamiri zao, upendo wao kwa Mungu utakuwa dhaifu. Ukizungumza tu kuhusu kulipa neema na upendo wa Mungu, hutakuwa na msukumo wowote katika upendo wako Kwake; kumpenda Yeye kwa kutegemea hisia za dhamiri yako ni mtazamo baridi. Ni kwa nini Nasema kwamba ni mtazamo baridi? Hili ni suala la utendaji. Huu ni upendo wa aina gani? Huku si kujaribu kumdanganya Mungu na kufanya kitu kwa namna isiyo ya dhati tu kwa ajili

Yake? Watu wengi sana huamini kwamba hakuna tuzo la kumpenda Mungu, na mtu ataadhibiwa hata hivyo kwa kutompenda Yeye, kwa hiyo kwa jumla kutotenda dhambi tu kunatosha. Kwa hiyo kumpenda Mungu na kulipa upendo Wake kwa kutegemeza hisia za dhamiri ya mtu ni mtazamo baridi, na si upendo kwa Mungu unaokuja kwa hiari kutoka moyoni mwa mtu. Upendo kwa Mungu unapaswa kuwa hisia halisi kutoka katika kina cha moyo wa mtu. Watu wengine husema: “Mimi mwenyewe niko radhi kumfuatilia Mungu na kumfuata Yeye. Sasa Mungu anataka kuniacha lakini bado nataka kumfuata Yeye. Iwapo Ananitaka au la, bado nitampenda Yeye, na mwishowe lazima nimpate Yeye. Ninatoa moyo wangu kwa Mungu, na haijalishi kile Yeye hufanya, nitamfuata Yeye kwa maisha yangu yote. Lolote litokealo, lazima nimpende Mungu na lazima nimpate Yeye; sitapumzika mpaka nimpate Yeye.” Una aina hii ya nia?

Njia ya kuamini katika Mungu ni njia ya kumpenda Yeye. Ikiwa unaamini katika Yeye lazima umpende Yeye; kwa hali yoyote, kumpenda Yeye hakuhusu tu kulipa upendo Wake au kumpenda kwa kutegemea hisia za dhamiri—ni pendo safi kwa Mungu. Kuna nyakati ambazo watu hutegemea tu dhamiri zao na hawawezi kuhisi upendo wa Mungu. Kwa nini kila mara Nilisema: “Roho wa Mungu asisimue roho zetu”? Kwa nini Sikuzungumzia kulisimua dhamiri za watu kumpenda Mungu? Ni kwa sababu dhamiri za watu haziwezi kuhisi kupendeza kwa Mungu. Ikiwa hujaridhishwa na maneno hayo, huenda ukatumia dhamiri yako kuhisi upendo Wake, na utakuwa na msukumo fulani wakati huo lakini baadaye utatoweka. Ukitumia tu dhamiri yako kuhisi kupendeza kwa Mungu, una msukumo unapoomba, lakini baadaye unaondoka tu, unatoweka. Hilo linahusu nini? Ukitumia tu dhamiri yako hutaweza kuamsha upendo wako kwa Mungu; unapohisi kweli kupendeza Kwake ndani ya moyo wako roho yako itasisimuliwa na Yeye, na ni wakati huo tu ndio dhamiri yako itaweza kufanya kazi yake ya asili. Hiyo ni kusema kwamba watu wakishasisimuliwa na Mungu katika roho zao na wakati roho zao zimepata maarifa na himizo, yaani, baada ya wao kupata uzoefu, ndipo tu wataweza kumpenda Mungu kwa kufaa na dhamiri zao. Kumpenda Mungu na dhamiri yako si vibaya—hiki ni kiwango cha chini sana cha kumpenda Mungu. Njia ya wanadamu ya upendo ya kufanya haki kwa shida tu kwa neema ya Mungu bila shaka haiwezi kuchochea kuingia kwao kiutendaji. Watu wanapopata baadhi ya kazi ya Roho Mtakatifu, yaani, wanapona na kuonja upendo wa Mungu katika uzoefu wao wa vitendo, wakiwa na maarifa fulani ya Mungu na kuona kweli kwamba Mungu anastahili sana upendo wa wanadamu na jinsi Alivyo mzuri, ni wakati huo tu ndio watu wanaweza kumpenda Mungu kwa uhalisi.

Watu wanapowasiliana na Mungu na mioyo yao, mioyo yao inapoweza kumgeukia Yeye kikamilifu, hii ni hatua ya kwanza ya upendo wa wanadamu kwa Mungu. Ikiwa unataka kumpenda Mungu, lazima kwanza uweze kugeuza moyo wako Kwake. Kugeuza moyo wako kwa Mungu ni nini? Ni wakati ambapo kila kitu unachofuatilia ndani ya moyo wako ni kwa ajili

ya kumpenda na kumpata Mungu, na hii inaonyesha kwamba umegeuza moyo wako kikamilifu kwa Mungu. Bali na Mungu na maneno Yake, hakuna takriban kitu chochote kingine ndani ya moyo wako (familia, mali, mume, mke, watoto au vitu vingine). Hata kama vipo, haviwezi kuumiliki moyo wako, na hufikirii juu ya matazamio yako ya baadaye lakini unafuatilia tu kumpenda Mungu. Wakati huo utakuwa umegeuza moyo wako kwa Mungu kabisa. Ikiwa bado unajitengenezea mipango ndani ya moyo wako na kila mara unafuatilia manufaa yako binafsi, na kila mara unafikiri: “Ni lini ninaweza kumwomba Mungu ombi ndogo? Familia yangu itakuwa tajiri lini? Ninawezaje kupata mavazi kadhaa mazuri? ...” Ikiwa unaishi katika hali hiyo inaonyesha kwamba moyo wako haujamgeukia Mungu kwa ukamilifu. Ikiwa una maneno ya Mungu tu moyoni mwako na unaweza kumwomba Mungu na kuwa karibu naye nyakati zote, kana kwamba Yeye yu karibu sana nawe, kana kwamba Mungu yu ndani yako nawe u ndani Yake, ikiwa uko katika hali ya aina hiyo, inamaanisha kwamba moyo wako umekuwa katika uwepo wa Mungu. Ukimwomba Mungu na kula na kunywa maneno Yake kila siku, unafikiria kila mara kuhusu kazi ya kanisa, ukifikiria juu ya mapenzi ya Mungu, ukitumia moyo wako kumpenda Yeye kwa uhalisi na kuridhisha moyo Wake, basi moyo wako utakuwa wa Mungu. Ikiwa moyo wako unamilikiwa na vitu vingine vingi, basi bado unamilikiwa na Shetani na haujamrudia Mungu kweli. Wakati moyo wa mtu umemrudia Mungu kweli, atakuwa na upendo halisi, wa hiari Kwake na ataweza kufikiria kazi ya Mungu. Ingawa bado atakuwa na hali za kipumbavu na zisizo na akili, ataweza kuwa na fikira kwa ajili ya maslahi ya nyumba ya Mungu, ya kazi Yake, na ya mabadiliko katika tabia yake. Moyo wake utakuwa sahihi kabisa. Watu wengine kila mara hupeperusha bendera ya kanisa haijalishi wanachofanya; kweli ni kwamba hii ni kwa manufaa yao. Mtu wa aina hiyo hana aina nzuri ya nia. Yeye ni mhalifu na mdanganyifu na mambo mengi sana anayofanya ni ya kutafuta manufaa yake mwenyewe. Mtu wa aina hiyo hafuatilii kumpenda Mungu; moyo wake bado ni wa Shetani na hauwezi kumgeukia Mungu. Mungu hana njia ya kumpata mtu wa aina hiyo.

Hatua ya kwanza ya kumpenda Mungu kweli na kupatwa na Yeye ni kuurudisha moyo wako kwa ukamilifu kwa Mungu. Katika kila jambo ufanyalo, jichunguze na uulize: “Ninafanya hiki kulingana na moyo wa upendo kwa Mungu? Kuna nia yoyote ya kibinafsi ndani yake? Lengo langu halisi la kufanya hili ni lipi?” Ikiwa unataka kumpa Mungu moyo wako lazima kwanza uuhini moyo wako, uachane na nia zako zote, na ufikie kiwango cha kuwa wa Mungu kwa ukamilifu. Hii ni njia ya kufanya mazoezi ya kumpa Mungu moyo wako. Kuuhini moyo wa mtu kunahusu nini? Ni kuachana na tamaa za kupita kiasi za mwili wa mtu, kutotamani baraka za cheo au kutamani starehe, kufanya kila kitu kumridhisha Mungu, na kwamba moyo wa mtu unaweza kuwa Wake kwa ukamilifu, sio kwa ajili ya mtu mwenyewe. Hivyo ndivyo ilivyo.

Upendo halisi kwa Mungu hutoka ndani ya kina cha moyo; ni upendo uliopo tu kwa msingi

wa wanadamu kumfahamu Mungu. Moyo wa mtu unapomgeukia Mungu kwa ukamilifu basi ana upendo kwa Mungu, lakini upendo huo sio lazima uwe takatifu na sio lazima uwe kamili. Hii ni kwa sababu kuna umbali fulani kati ya moyo wa mtu kumgeukia Mungu kwa ukamilifu na mtu huyo kuwa na ufahamu halisi wa Mungu na kuabudu kihalisi Kwake. Njia ya mtu kutimiza upendo wa kweli kwa Mungu na kujua tabia ya Mungu ni kuurudisha moyo wake kwa Mungu. Baada ya kutoa moyo wao wa kweli kwa Mungu, wataanza kuingia katika uzoefu wa maisha, na hivyo tabia yao itaanza kubadilika, upendo wao kwa Mungu utakua polepole, na ufahamu wao wa Mungu utaongezeka pia polepole. Kwa hivyo kuurudisha moyo wa mtu kwa Mungu ni sharti la mwanzo la kuingia katika njia sahihi ya uzoefu wa maisha. Watu wanapoweka mioyo yao mbele ya Mungu, wao huwa tu na moyo wa kumtamani Yeye lakini sio wa kumpenda Yeye, kwa sababu hawana ufahamu kumhusu Yeye. Hata ingawa katika hali hii wana upendo fulani Kwake, si wa hiari na si halisi. Hii ni kwa sababu chochote kitokacho kwa mwili wa mwanadamu ni athari ya kihisia na hakitoki kwa ufahamu halisi. Ni msukumo wa muda mfupi tu na hakiwezi kuwa ibada ya kudumu. Watu wasipokuwa na ufahamu wa Mungu wanaweza tu kumpenda Yeye kulingana na upendeleo wao wenyewe na fikira zao binafsi; aina hiyo ya upendo haiwezi kuitwa upendo wa hiari, wala haiwezi kuitwa upendo halisi. Moyo wa mtu ukimrudia Mungu kwa uhalisi, anaweza kufikiria juu ya maslahi ya Mungu katika kila kitu, lakini ikiwa hana ufahamu wowote wa Mungu, hana uwezo wa kuwa na upendo wa hiari kwa uhalisi. Yote anayoweza kufanya ni kutimiza kazi fulani za kanisa na kutekeleza wajibu wake mdogo, lakini hauna msingi. Mtu wa aina hiyo ana tabia ambayo ni ngumu kubadilisha; wao wote ni watu ambao ama hawaufuatilia ukweli, au hawauielewi. Hata mtu akiurudisha kabisa moyo wake kwa Mungu haimaanishi kwamba moyo wake wa upendo kwa Mungu ni safi kabisa, kwa sababu wale walio na Mungu ndani ya mioyo yao sio lazima kwamba wanao upendo ndani ya mioyo yao kwa Mungu. Hili linahusu utofautishaji kati ya mtu anayefuatilia au asiyefuatilia ufahamu wa Mungu. Mara tu mtu anapokuwa na ufahamu wa Yeye, inaonyesha kwamba moyo wake umemrudia Mungu kwa ukamilifu, inaonyesha kwamba upendo wake halisi kwa Mungu ndani ya moyo wake ni wa hiari. Mtu wa aina hiyo pekee ndiye ana Mungu ndani ya moyo wake. Kugeuza moyo wa mtu kwa Mungu ni sharti la mwanzo la yeye kuingia katika njia sahihi, la kumfahamu Mungu, na la kutimiza upendo wa Mungu. Siyo alama ya kukamilisha wajibu wake ya kumpenda Mungu, wala siyo alama ya kuwa na upendo halisi Kwake. Njia ya pekee ya mtu kutimiza upendo halisi kwa Mungu ni kuurudisha moyo wake kwa Mungu, ambacho pia ni kitu cha kwanza mmoja wa uumbaji Wake anapaswa kufanya. Wale wanaompenda Mungu wote ni watu wanaotafuta uzima, yaani, watu wanaofuatilia ukweli na watu wanaomtaka Mungu kweli; wote wana nuru ya Roho Mtakatifu na wamesisimuliwa na Yeye. Wote wanaweza kuongozwa na Mungu.

Mtu anapoweza kuhisi kwamba ni mdeni wa Mungu ni kwa sababu amesisimuliwa na Roho; akihisi hivyo basi ataelekea kuwa na moyo wa kutamani na ataweza kufuatilia kuingia katika maisha. Lakini ukiachia katika hatua fulani, hutaweza kuingia ndani zaidi; bado kuna hatari kubwa ya kukwama katika wavu wa Shetani, na ikifikia kiwango fulani utatekwa nyara na Shetani. Mwangaza wa Mungu huwaruhusu watu kujijua na baadaye kuhisi kuwa kwao na deni kwa Mungu pamoja na kuwa radhi kushirikiana naye na kutupilia mbali mambo yasiyomfurahisha Yeye. Hii ni kanuni ya kazi ya Mungu. Nyote mko radhi kufuatilia kukua katika maisha yenu na kumpenda Mungu, kwa hiyo umejiondolea njia zako za kubabiababia? Ukijiondolea njia hizo tu na usisababishe vurugu yoyote au kujionyesha, hiyo kweli ni kufuatilia kukua katika maisha yako? Ikiwa huna mienendo yoyote ya juujuu lakini huingii katika maneno ya Mungu, inamaanisha kwamba wewe ni mtu asiye na maendeleo yoyote ya utendaji. Ni nini mzizi wa kutwaa mwenendo wa juujuu? Je, matendo yako ni kwa ajili ya kukua katika maisha yako? Unafuatilia kustahili kuwa mmoja wa watu wa Mungu? Chochote kile unacholenga ndicho utakachoishi kwa kudhihirisha; ukilenga njia za juujuu basi moyo wako unalenga nje, na hutakuwa na njia ya kufuatilia kukua katika maisha yako. Mungu anataka mabadiliko katika tabia, lakini kila mara unafuatilia mambo ya nje; mtu wa aina hii hatakuwa na njia ya kubadilisha tabia yake! Kila mtu ana njia fulani kabla ya kukomaa katika maisha yake, ambayo ni kuwa lazima akubali hukumu, kuadibu, na kukamilishwa kwa maneno ya Mungu. Ikiwa huna maneno ya Mungu lakini unategemea tu kujiamini kwako na nia, kila kitu ufanyacho kinategemea ari. Yaani, ikiwa unataka ukuaji katika maisha yako lazima ule na kunywa, na ufahamu zaidi maneno ya Mungu. Wote wanaofanywa wakamilifu na maneno Yake wanaweza kuishi kwa kuyadhihirisha; wale wasiopitia usafishaji wa maneno Yake, wasiopitia hukumu ya maneno Yake hawawezi kufaa kwa matumizi Yake. Kwa hiyo mnaishi kwa kudhihirisha maneno Yake kwa kiwango gani? Mkila na kunywa tu maneno ya Mungu na muweze kuyalinganisha kwa hali yenu ya maisha, na kupata njia ya kutenda kwa kuzingatia masuala ninayotaja ndipo kutenda kwenu kutakuwa sahihi. Pia kutakuwa kwa kuupendeza moyo wa Mungu. Mtu aliye na aina hii ya kutenda pekee ndiye aliye na nia ya kumpenda Mungu.

Kuhusu Desturi ya Sala

Nyinyi hamtilii maanani sala katika maisha yenu ya kila siku. Watu daima wamepuuza sala. Hapo awali sala zilikuwa za uzembe, huku mwanadamu akifanya tu mambo kwa namna isiyo ya dhati mbele za Mungu. Hakuna mwanadamu aliyeutoa moyo wake kwa ukamilifu mbele ya Mungu na alifanya sala ya kweli kwa Mungu. Mwanadamu alimwomba tu Mungu wakati ambapo tatizo lilitokea. Katika wakati huu wote, umewahi kweli kumwomba Mungu? Je, umewahi kutoa machozi ya uchungu mbele ya Mungu? Je, umewahi kujijua mwenyewe mbele ya Mungu? Je, umewahi kumwomba Mungu maombi ya kutoka? Sala huja kupitia kufanya

mazoezi: Ikiwa kwa kawaida huombi nyumbani, basi hutakuwa na njia yoyote ya kuomba kanisani, na kama kwa kawaida huombi wakati wa mikusanyiko midogo, basi hutaweza kusali wakati wa mikusanyiko mikubwa. Ikiwa kwa kawaida humkaribii Mungu au kutafakari juu ya maneno ya Mungu, basi hutakuwa na chochote cha kusema wakati wa kuomba—na hata kama utaomba, utakuwa tu unaunga mkono kwa maneno matupu; hutakuwa unaomba kwa kweli.

Ni nini maana ya kuomba kwa kweli? Ina maana ya kuzungumza maneno yaliyo ndani ya moyo wako kwa Mungu, na kuwasiliana na Mungu baada ya kufahamu mapenzi Yake na kutegemea maneno Yake; ina maana ya kuhisi kuwa karibu na Mungu hasa, kuhisi kwamba Yeye yuko mbele yako, na kwamba una kitu cha kumwambia; na inamaanisha kuwa mwangavu hasa ndani ya moyo wako, na kuhisi kwamba Mungu ni wa kupendeza hasa. Utajisikia kutiwa moyo sana, na baada ya kusikia maneno yako ndugu zako watajisikia kufurahishwa, watahisi kwamba maneno unayosema ni maneno yaliyo ndani ya mioyo yao, maneno ambayo wangependa kusema, na kwamba kile unachosema kinawakilisha kile wanachotaka kusema. Hii ndiyo maana ya kuomba kwa kweli. Baada ya kuomba kwa kweli, moyoni mwako utahisi kuwa na amani, na kufurahishwa; nguvu ya kumpenda Mungu itaongezeka, na utahisi kwamba hakuna kitu chochote katika maisha yako yote kinachostahili au ni muhimu zaidi kuliko kumpenda Mungu—na yote haya yatathibitisha kuwa maombi yako yamekuwa yenye ufanisi. Je, umewahi kuomba kwa njia hiyo?

Na je, kuhusu maudhui ya sala? Unapaswa kuomba, hatua kwa hatua, kwa mujibu wa hali yako ya kweli na kile kinachotakiwa kufanywa na Roho Mtakatifu, na unapaswa kuwasiliana kwa karibu na Mungu kulingana na mapenzi ya Mungu na mahitaji Yake kwa mwanadamu. Unapoanza kufanya mazoezi ya maombi yako, kwanza peana moyo wako kwa Mungu. Usijaribu kufahamu mapenzi ya Mungu; jaribu tu kuzungumza maneno yaliyo ndani ya moyo wako kwa Mungu. Unapokuja mbele za Mungu, sema hivi: “Ee Mungu! Leo tu ndio natambua kuwa nilikuwa nikikuasi. Mimi kweli ni mpotovu na mwenye kustahili dharau. Awali, nilikuwa nikipoteza muda wangu; kuanzia leo nitaishi kwa ajili Yako, nitaishi kwa kudhihirisha maisha ya maana, na kuridhisha mapenzi Yako. Ningependa Roho Wako afanye kazi ndani yangu daima, na daima aniangaze na kunipa nuru, ili nipate kuwa na ushuhuda wenye nguvu na unaosikika mbele Zako, unaomruhusu Shetani kuuona utukufu Wako, ushuhuda Wako, na thibitisho la ushindi Wako ndani yetu.” Wakati unapoomba kwa njia hii, moyo wako utawekwa huru kabisa, baada ya kuomba kwa njia hii, moyo wako utakuwa karibu na Mungu, na kwa kuomba hivi mara kwa mara, Roho Mtakatifu atafanya kazi ndani yako bila shaka. Ikiwa daima wewe humwita Mungu kwa njia hii na kufanya azimio lako mbele ya Mungu, siku itawadia ambapo azimio lako litaweza kukubalika mbele ya Mungu, wakati moyo wako na nafsi yako vyote vitapokelewa na Mungu, na hatimaye utakamilishwa na Mungu. Sala ni ya muhimu sana kwenu. Unapoomba,

unapokea kazi ya Roho Mtakatifu, hivyo moyo wako unaguswa na Mungu, na nguvu za upendo kwa Mungu ndani yako huchipuka. Ikiwa hutaomba kwa moyo wako, ikiwa hutafungua moyo wako kuwasiliana kwa karibu na Mungu, basi Mungu hatakuwa na njia ya kufanya kazi ndani yako. Ikiwa, baada ya kusali, umesema maneno yote yaliyo ndani ya moyo wako na Roho wa Mungu hajafanya kazi, ikiwa huhisi kutiwa moyo ndani, basi hili linaonyesha kwamba moyo wako hauna ari, kwamba maneno yako si ya kweli, na bado wewe ni mchafu. Ikiwa, baada ya kusali, unafurahishwa, basi sala zako zimekubaliwa na Mungu na Roho wa Mungu amefanya kazi ndani yako. Kama mtu ambaye huhudumu mbele ya Mungu, huwezi kuwa bila sala. Ikiwa unaona ushirika na Mungu kama kitu ambacho kina maana na cha thamani, ungeweza kuacha sala? Hakuna mtu anayeweza kuwa bila mawasiliano ya karibu na Mungu. Bila sala, unaishi katika mwili, unaishi katika utumwa wa Shetani; bila sala ya kweli, unaishi chini ya ushawishi wa giza. Natumaini kwamba ndugu wanaweza kuomba kila siku. Huku si kuzingatia mafundisho ya dini, hata hivyo, bali matokeo ambayo yanapaswa kutimizwa. Je, uko tayari kuacha usingizi kidogo na anasa, kusema sala za asubuhi wakati wa alfajiri na kisha kufurahia maneno ya Mungu? Ukiomba kwa moyo safi na kula na kunywa maneno ya Mungu hivi, utakubalika zaidi Kwake. Ukifanya hivi kila asubuhi, ukifanya mazoezi ya kumpa Mungu moyo wako kila siku na kuwasiliana kwa karibu na Mungu, basi ufahamu wako wa Mungu utaongezeka bila shaka, na utaweza kufahamu vizuri zaidi mapenzi ya Mungu. Unapaswa kusema: “Ee Mungu! Ningependa kutimiza wajibu wangu. Ili Uweze kutukuzwa ndani yetu, na Uweze kufurahia ushuhuda ulio ndani yetu, kikundi hiki cha watu, naweza tu kutoa nafsi yangu yote kwako. Nakuomba Ufanye kazi ndani yetu, ili niweze kukupenda na kukuridhisha kwa kweli, na kukufanya Uwe lengo ambalo ninafuatilia.” Wakati ambapo unakuwa na mzigo huu, Mungu atakufanya uwe mkamilifu bila shaka; hupaswi tu kuomba kwa ajili yako mwenyewe, bali pia kwa ajili ya kufanya mapenzi ya Mungu, na kwa ajili ya kumpenda Yeye. Hiyo ndiyo aina ya sala ya kweli kabisa. Je, wewe huomba ili kutenda mapenzi ya Mungu?

Hapo awali, nyinyi hamkujua jinsi ya kuomba, na mlipuuza maombi; leo, lazima mjitahidi kabisa kujifundisha kuomba. Ikiwa huwezi kuwa na ujasiri wa kumpenda Mungu, basi unawezaje kuomba? Unapaswa kusema: “Ee Mungu! Moyo wangu hauwezi kukupenda kweli, nataka kukupenda lakini sina nguvu. Napaswa kufanya nini? Napenda Ufungue macho ya roho yangu, napenda Roho Wako auguse moyo wangu, ili mbele Yako nivuliwe hali zote za kutoonyesha hisia, na nisishurutishwe na mtu yeyote, jambo, au kitu; nauweka moyo wangu wazi kabisa mbele Yako, ili nafsi Yangu yote ijitoe mbele Yako, na Uweze kunijaribu vile Utakavyo. Sasa, siwazii matarajio yangu, wala sifungwi na kifo. Kwa kuutumia moyo wangu ambao unakupenda, napenda kutafuta njia ya uzima. Vitu vyote na matukio viko mikononi Mwako, majaliwa yangu yako mikononi Mwako, na, zaidi ya hayo, maisha yangu yanadhibitiwa na

mikono Yako. Sasa, nafuatilia kukupenda Wewe, na bila kujali kama Wewe unaniruhusu kukupenda, haijalishi jinsi Shetani anavyoingilia, nimeamua kukupenda Wewe.” Unapokabiliwa na mambo kama hayo, unasali kwa njia hii. Ikiwa utafanya hivyo kila siku, nguvu ya kumpenda Mungu itaongezeka polepole.

Mtu huingiaje katika sala ya kweli?

Unapoomba, lazima uwe na moyo ambao ni mtulivu mbele ya Mungu, na lazima uwe na moyo mwaminifu. Wewe kweli unawasiliana kwa karibu na kuomba na Mungu—usimdanganye Mungu kwa kutumia maneno ya kupendeza. Sala lazima ilenge kile ambacho Mungu anataka kukamilisha leo. Mwombe Mungu akupe nuru na mwangaza mwingi zaidi, na ulete hali halisi na matatizo yako mbele za Mungu kuomba, na ufanye azimio mbele za Mungu. Sala sio kufuata utaratibu, bali ni kumtafuta Mungu kwa kutumia moyo wako wa kweli. Omba kwamba Mungu aulinde moyo wako, na Aufanye uwe na amani mara nyingi mbele za Mungu, Akuwezeshe kujijua, na kujidharau, na kujitupa katika mazingira ambayo Mungu amekuwekea, hivyo kukuruhusu uwe na uhusiano wa kawaida na Mungu na kukufanya mtu anayempenda Mungu kweli.

Ni nini umuhimu wa sala?

Sala ni mojawapo ya njia ambazo mwanadamu hutumia kushirikiana na Mungu, ni njia ambayo mwanadamu hutumia kumwita Mungu, na ni mchakato ambao mtu huguswa na Roho wa Mungu. Inaweza kusemwa kwamba wale ambao hawana sala ni wafu wasio na roho, ushahidi kwamba hawana uwezo wa kuguswa na Mungu. Bila sala, watu hawawezi kupata maisha ya kawaida ya kiroho, sembuse kuifuata kazi ya Roho Mtakatifu; bila sala, wao huvunja uhusiano wao na Mungu, na hawawezi kupokea kibali cha Mungu. Ukiwa mtu anayemwamini Mungu, kadri unavyoomba, ndivyo unavyozidi kuguswa na Mungu. Watu kama hao wana azimio kubwa zaidi na wanaweza kupokea zaidi nuru ya hivi karibuni kutoka kwa Mungu; kwa hivyo, watu kama hawa pekee ndio wanaweza kukamilishwa mapema iwezekanavyo na Roho Mtakatifu.

Je, ni matokeo gani yanayofaa kutimizwa kwa sala?

Watu wanaweza kutekeleza mazoea ya sala na kuelewa umuhimu wa sala, lakini matokeo yanayofaa kutimizwa kwa sala sio jambo rahisi. Sala sio jambo la kupitia urasmi wa kisheria, au kufuata utaratibu, au kukariri maneno ya Mungu, ambalo ni kusema, sala haimaanishi kuiga maneno kama kasuku na kuwaiga wengine. Katika sala, lazima umpe Mungu moyo wako, ukishiriki maneno yaliyo ndani ya moyo wako na Mungu ili uweze kuguswa na Mungu. Ikiwa maombi yako yatakuwa na matokeo, basi lazima yategemee usomaji wako wa maneno ya Mungu. Ni kwa kuomba tu katikati ya maneno ya Mungu ndipo utaweza kupokea nuru na

mwangaza zaidi. Sala ya kweli huonyeshwa kwa kuwa na moyo ambao unatamani sana matakwa yaliyowekwa na Mungu, na kuwa tayari kutimiza matakwa haya; utaweza kuchukua yote ambayo Mungu huchukua, kwa msingi huo utakuwa na maarifa, na utajua na kuelewa wazi kuhusu ukweli ulioelezwa na Mungu. Kuwa na azimio, na imani, na maarifa, na njia ya kufanya mazoezi baada ya kuomba—huku tu ndiko kuomba kwa kweli, na sala kama hii tu ndiyo inaweza kuwa na ufanisi. Lakini sala lazima ijengwe juu ya msingi wa kufurahia maneno ya Mungu na kuwasiliana kwa karibu na Mungu katika maneno Yake, moyo wako ukiweza kumtafuta Mungu na kuwa na amani mbele ya Mungu. Sala kama hiyo tayari imefikia kiwango cha kuwasiliana kwa kweli na Mungu.

Maarifa ya msingi kuhusu kuomba:

1. Usiseme kijinga chochote kinachokuja kwenye akili. Lazima kuwe na mzigo ndani ya moyo wako, ambalo ni kusema, lazima uwe na lengo wakati unapoomba.

2. Sala lazima iwe na maneno ya Mungu; lazima itegemezwe kwa maneno ya Mungu.

3. Wakati unapoomba, ni sharti usitumie tena masuala yaliyopitwa na wakati. Maombi Yako yanapaswa kuhusiana na maneno ya sasa ya Mungu, na unapoomba, umwambie Mungu mawazo yako ya ndani kabisa.

4. Sala ya kikundi inapaswa kulenga kiini, ambacho lazima kiwe kazi ya Roho Mtakatifu leo.

5. Watu wote lazima wajifunze sala ya kuombea. Hii pia ni njia ya kuyadhukuru mapenzi ya Mungu.

Maisha ya maombi ya kibinafsi yanategemea kuelewa umuhimu wa sala na maarifa ya msingi ya sala. Katika maisha ya kila siku, omba mara kwa mara kwa ajili ya dosari zako, omba upate mabadiliko katika tabia yako maishani, na omba kwa msingi wa maarifa yako ya maneno ya Mungu. Kila mtu anapaswa kuanzisha maisha yake ya maombi, anapaswa kuombea maarifa kutegemea maneno ya Mungu, anapaswa kuomba ili kutafuta maarifa ya kazi ya Mungu. Weka hali zako za kweli mbele ya Mungu, na uwe wa vitendo, na usitilie maanani mbinu; la muhimu ni kupata maarifa ya kweli, na kupata maneno ya Mungu kwa kweli. Yeyote anayefuatilia kuingia katika maisha ya kiroho lazima aweze kuomba kwa njia nyingi. Sala ya kimya, kutafakari maneno ya Mungu, kuja kuijua kazi ya Mungu, na kadhalika—kazi hii inayolengwa ya kuwasiliana kwa karibu, ni ili kutimiza kuingia katika maisha ya kawaida ya kiroho, kuifanya hali yako mwenyewe mbele za Mungu iwe bora zaidi, na kusababisha maendeleo makubwa zaidi katika maisha yako. Kwa kifupi, yote unayoyafanya—kama ni kula na kunywa maneno ya

Mungu, au kuomba kimya au kutangaza kwa sauti—ni ili kuona wazi maneno ya Mungu, na kazi Yake, na kile Anachotaka kutimiza ndani yako. La muhimu zaidi, ni ili kufikia viwango ambavyo Mungu anahitaji na kuyapeleka maisha yako kwa kiwango kinachofuata. Kiwango cha chini zaidi ambacho Mungu anahitaji kwa watu ni kwamba waweze kufungua mioyo yao Kwake. Ikiwa mwanadamu atautoa moyo wake wa kweli kwa Mungu na kusema kile kilicho ndani ya moyo wake kwa Mungu, basi Mungu yuko tayari kufanya kazi ndani ya mwanadamu; Mungu hataki moyo wa mwanadamu uliopotoka, lakini moyo wake ulio safi na mwaminifu. Ikiwa mwanadamu hasemi yaliyo moyoni mwake kwa Mungu kwa kweli, basi Mungu haugusi moyo wa mwanadamu, au kufanya kazi ndani yake. Hivyo, jambo muhimu sana kuhusu kuomba ni kusema maneno ya moyo wako wa kweli kwa Mungu, kumwambia Mungu kuhusu dosari zako au tabia ya kuasi na kujifungua kabisa kwa Mungu. Wakati huo tu ndipo Mungu atakuwa na hamu ya sala zako; la sivyo, basi Mungu atauficha uso Wake kutoka kwako. Kigezo cha chini kabisa cha sala ni kwamba lazima uweze kuuweka moyo wako kwa amani mbele za Mungu, na hupaswi kuondoka kwa Mungu. Pengine, wakati huu, hujapata mtazamo mpya au wa juu, lakini lazima utumie sala ili mambo yaendeleo kama yalivyo—huwezi kurudi nyuma. Hili ndilo jambo dogo zaidi ambalo unapaswa kutimiza. Ikiwa huwezi kufanikisha hata hili, basi inathibitisha kwamba maisha yako ya kiroho hayajaingia katika njia sahihi; kwa hiyo, huwezi kushikilia maono yako ya mwanzo, na kuondolea imani kwa Mungu, na uamuzi wako hatimaye hutoweka. Kuingia kwako katika maisha ya kiroho kunadhihirishwa na iwapo sala zako zimeingia katika njia sahihi au la. Watu wote lazima waingie katika uhalisi huu, lazima wafanye kazi ya kujifunza wenyewe kwa kufahamu katika sala, sio kusubiri kwa kukaa tu, lakini kwa ufahamu watafute kuguswa na Roho Mtakatifu. Wakati huo tu ndipo watakuwa watu wanaomtafuta Mungu kwa kweli.

Unapoanza kuomba, lazima uwe mwenye uhalisi, na usitake kufanya kupita kiasi; huwezi kufanya madai ya ubadhirifu, ukitumaini kwamba mara tu utakapofungua kinywa chako utaguswa na Roho Mtakatifu, utapata nuru na mwangaza, na kupewa neema nyingi. Hilo haliwezekani—Mungu hafanyi mambo yaliyo ya rohoni. Mungu hutimiza sala za watu kwa wakati Wake mwenyewe na wakati mwingine Yeye hujaribu imani yako kuona kama wewe ni mwaminifu mbele Zake. Unapoomba lazima uwe na imani, uvumilivu, na azimio. Watu wengi wanapoanza kujifunza kuomba, hawahisi kuwa wameguswa na Roho Mtakatifu na hivyo huvunjika moyo. Hili halikubaliki! Lazima uwe na nia ya kutobadili msimamo, lazima ulenge kuhisi mguso wa Roho Mtakatifu, na kutafuta na kuchunguza. Wakati mwingine, njia unayofuata ni ile isiyo sahihi; wakati mwingine, misukumo na dhana zako haviwezi kusimama imara mbele za Mungu, na hivyo Roho wa Mungu hakusisimui; vivyo pia kuna nyakati ambapo Mungu huangalia kama wewe ni mwaminifu au la. Kwa kifupi, lazima ujitahidi zaidi katika kujifunza.

Ikiwa utatambua kuwa njia unayoifuata ni ya kuacha maadili, unaweza kubadilisha jinsi unavyoomba. Maadamu unatafuta kwa kweli, na unatamani kupokea, basi Roho Mtakatifu atakuingiza kwenye ukweli huu. Wakati mwingine unasali kwa moyo wa ukweli lakini huhisi kama umeguswa hasa. Katika nyakati kama hizi lazima utegemee imani yako, na uamini kwamba Mungu anayaangalia maombi yako; lazima uwe na uvumilivu katika sala zako.

Lazima uwe mwaminifu, na lazima uombe ili uondoe ujanja ndani ya moyo wako. Unapotumia maombi ili kujitakasa wakati wowote inapohitajika, na kuyatumia ili uguswe na Roho wa Mungu, tabia yako itabadilika polepole. Maisha ya kweli ya kiroho ni maisha ya sala, na ni maisha ambayo yanaguswa na Roho Mtakatifu. Mchakato wa kuguswa na Roho Mtakatifu ni mchakato wa kubadilisha tabia ya mwanadamu. Maisha ambayo hayajaguswa na Roho Mtakatifu si maisha ya kiroho, bado ni ibada ya kidini; wale tu ambao huguswa na Roho Mtakatifu mara kwa mara, na wamepewa nuru na kuangazwa na Roho Mtakatifu, ndio watu ambao wameingia katika maisha ya kiroho. Tabia ya mwanadamu hubadilika kwa uthabiti wakati anapoomba, na kadri anavyosisimuliwa na Roho wa Mungu, ndivyo anavyozidi kuwa hai na mtiifu. Kwa hiyo, pia, moyo wake utatakaswa polepole, baada ya hapo tabia yake itabadilika polepole. Hayo ndiyo matokeo ya sala ya kweli.

Jua Kazi Mpya Zaidi ya Mungu na Ufuate Nyayo Zake

Sasa, mnatakiwa kufuatilia kugeuka kuwa watu wa Mungu, na mtaanza kuingia kote katika njia sahihi. Kuwa watu wa Mungu kuna maana ya kuingia katika Enzi ya Ufalme. Leo, mnaanza rasmi kuingia katika mafunzo ya ufalme, na maisha yenu ya baadaye yatakoma kuwa goigoi na hobelahobela kama yalivyokuwa awali; maisha hayo ni yasiyoweza kufikia viwango vinavyotakiwa na Mungu. Kama huhisi umuhimu wowote, basi hili huonyesha kwamba huna hamu ya kujiendeleza mwenyewe, kwamba ukimbizaji wako umekanganywa na kuchanganywa, na wewe ni usiyeweza kutimiza mapenzi ya Mungu. Kuingia katika mafunzo ya ufalme kuna maana ya kuanza maisha ya watu wa Mungu—uko radhi kuyakubali mafunzo hayo? Uko radhi kuhisi kuthamini kwa umuhimu? Uko radhi kuishi chini ya nidhamu ya Mungu? Uko radhi kuishi chini ya kuadibu kwa Mungu? Wakati ambapo maneno ya Mungu yatakuja na kukujaribu, utafanyaje? Na utafanya nini wakati ambapo utakabiliwa na aina yote ya ukweli? Zamani, kulenga kwako hakukuwa juu ya maisha; leo, lazima uingie katika uhalisi wa maisha, na kufuatilia mabadiliko katika tabia ya maisha yako. Hili ndilo lazima litimizwe na watu wa ufalme. Wale wote ambao ni watu wa Mungu lazima wawe na uzima, lazima wakubali mafunzo ya ufalme, na kufuatilia mabadiliko katika tabia ya maisha yao. Hili ndilo Mungu huwashurutisha watu wa ufalme.

Masharti ya Mungu kwa watu wa ufalme ni kama yafuatayo:

1. Lazima wakubali maagizo ya Mungu, ambalo ni kusema, lazima wakubali maneno yote yaliyonenwa katika kazi ya Mungu ya siku za mwisho.

2. Lazima waingie katika mafunzo ya ufalme.

3. Lazima wafuatilie kufanya mioyo yao iguswe na Mungu. Wakati ambapo moyo wako umeelekea kwa Mungu kabisa, na una maisha ya kiroho ya kawaida, utaishi katika eneo la uhuru, ambalo lina maana kuwa utaishi chini ya utunzaji na ulinzi wa upendo wa Mungu. Ukiishi chini ya utunzaji na ulinzi wa Mungu tu ndipo utakuwa wa Mungu.

4. Lazima wapatwe na Mungu.

5. Lazima wawe dhihirisho la utukufu wa Mungu duniani.

Haya mawazo makuu matano ni maagizo Yangu kwenu. Maneno Yangu yananenwa kwa watu wa Mungu, na kama hutaki kuyakubali maagizo haya, Sitakulazimisha—lakini ukiyakubali kwa kweli, basi utaweza kuyafanya mapenzi ya Mungu. Leo, anzeni kuyakubali maagizo ya Mungu, na kufuatilia kuwa watu wa ufalme na kufikia viwango vinavyohitajika kuwa watu wa ufalme. Hii ndiyo hatua ya kwanza ya kuingia. Kama ungependa kufanya mapenzi ya Mungu kwa ukamilifu, basi lazima uyakubali maagizo haya matano, na kama unaweza kuyatimiza, utaupendeza moyo wa Mungu na kwa hakika utatumiwa sana na Mungu. Kilicho cha maana sana leo ni kuingia katika mafunzo ya ufalme. Kuingia katika mafunzo ya ufalme kunahusisha maisha ya kiroho. Awali, hakukuwa na mazungumzo ya maisha ya kiroho, lakini leo, unapoanza kuingia katika mafunzo ya ufalme, unaingia rasmi katika maisha ya kiroho.

Maisha ya kiroho ni maisha ya aina gani? Maisha ya kiroho ni yale ambayo kwayo moyo wako umeelekea kwa Mungu kabisa, na unaweza kuwa mzingatifu wa upendo wa Mungu. Ni yale ambayo kwayo unaishi katika maneno ya Mungu, na hakuna kingine kinachoushughulisha moyo wako, na unaweza kuyafahamu mapenzi ya Mungu leo, na unaongozwa na nuru ya Roho Mtakatifu leo ili kutimiza wajibu wako. Maisha kama hayo kati ya mwanadamu na Mungu ndiyo maisha ya kiroho. Kama huwezi kuifuata nuru ya leo, basi umbali umefunguka katika uhusiano wako na Mungu—huenda hata ukawa umevunjwa—na huna maisha ya kiroho ya kawaida. Uhusiano wa kawaida na Mungu hujengwa juu ya msingi wa kukubali maneno ya Mungu leo. Je, una maisha ya kiroho ya kawaida? Je, una uhusiano wa kawaida na Mungu? Wewe ni mtu anayeifuata kazi ya Roho Mtakatifu? Kama unaweza kufuata nuru ya Roho Mtakatifu leo, na unaweza kufahamu mapenzi ya Mungu ndani ya maneno Yake, na kuingia katika maneno haya, basi wewe ni mtu ambaye hufuata mkondo wa Roho Mtakatifu. Kama hufuati mkondo wa Roho Mtakatifu, basi wewe bila shaka ni mtu asiyefuatilia ukweli. Roho Mtakatifu hana nafasi ya kufanya kazi ndani ya wale ambao hawana hamu ya kujiendeleza wenyewe, na kutokana na

hayo, watu hao hawawezi kamwe kukusanya nguvu zao, na kila mara wao huwa baridi. Leo, wewe hufuata mkondo wa Roho Mtakatifu? Wewe uko ndani ya mkondo wa Roho Mtakatifu? Je, umeibuka kutoka kwa hali baridi? Wale wote ambao huamini katika maneno ya Mungu, ambao huchukulia kazi ya Mungu kama msingi, na hufuata nuru ya Roho Mtakatifu leo—wao wote wako ndani ya mkondo wa Roho Mtakatifu. Kama wewe huamini kwamba maneno ya Mungu ni kweli na sahihi kwa dhahiri, na kama wewe huamini maneno ya Mungu bila kujali kile Yeye husema, basi wewe ni mtu ambaye hufuatilia kuingia katika kazi ya Mungu, na kwa njia hii utatimiza mapenzi ya Mungu.

Ili kuingia katika mkondo wa Roho Mtakatifu lazima uwe na uhusiano wa kawaida na Mungu, na lazima kwanza ujiondoshe kwa hali yako baridi. Watu wengine kila mara hufuata walio wengi, na mioyo yao imetangatanga mbali sana na Mungu; watu hao hawana hamu ya kujiendeleza wenyewe, na viwango ambavyo wao hufuatilia ni vya chini sana. Ukimbizaji wa kumpenda Mungu tu na kupatwa na Mungu ndiyo mapenzi ya Mungu. Kuna watu ambao hutumia tu dhamiri yao kulipa mapenzi ya Mungu, lakini hili haliwezi kuridhisha mapenzi ya Mungu; kadri viwango unavyofuatilia vilivyo juu zaidi, ndivyo vitakavyokuwa vinawiana na mapenzi ya Mungu. Kama mtu aliye wa kawaida, na ambaye hufuatilia upendo wa Mungu, kuingia katika ufalme kuwa mmoja wa watu wa Mungu ni siku za usoni zenu za kweli, na maisha ambayo ni yenye thamani na maana sana; hakuna aliyebarikiwa kuliko ninyi. Mbona Nasema hili? Kwa sababu wale wasiomwamini Mungu huishi kwa ajili ya mwili, na wao huishi kwa ajili ya Shetani, lakini leo ninyi huishi kwa ajili ya Mungu, na huishi kufanya mapenzi ya Mungu. Ndiyo maana Nasema maisha yenu ni yenye maana sana. Ni kundi hili tu la watu, ambao wameteuliwa na Mungu, wanaweza kuishi kwa kudhihirisha maisha ya maana sana: Hakuna mwingine duniani anaweza kuishi kwa kudhihirisha maisha ya thamani na maana hivyo. Kwa sababu mmeteuliwa na Mungu, na mmekuzwa na Mungu, na, aidha, kwa sababu ya upendo wa Mungu kwenu, mmefahamu uzima wa kweli, na mnajua namna ya kuishi maisha yenye thamani sana. Hili si kwa sababu ukimbizaji wenu ni mzuri, lakini kwa sababu ya neema ya Mungu; ni Mungu aliyefungua macho ya roho zenu, na ni Roho wa Mungu aliyegusa mioyo yenu, kuwapa ninyi bahati nzuri ya kuja mbele Yake. Kama Roho wa Mungu hangekuwa amekupa nuru, basi hungekuwa na uwezo wa kuona kilicho cha kupendeza kuhusu Mungu, wala haingewezekana kwa wewe kumpenda Mungu. Ni kwa sababu kabisa Roho wa Mungu amegusa mioyo ya watu ndiyo mioyo yao imeelekea kwa Mungu. Mara nyingine, wakati ambapo unafurahia maneno ya Mungu, roho yako huguswa, na wewe huhisi kwamba huna budi kumpenda Mungu, kwamba kuna nguvu nyingi ndani yako, na kwamba hakuna chochote usichoweza kuweka kando. Kama wewe unahisi hivi, basi umeguswa na Roho wa Mungu, na moyo wako umeelekea kwa Mungu kabisa, na utamwomba Mungu na kusema: “Ee Mungu! Sisi

kweli tumejaaliwa na kuteuliwa na Wewe. Utukufu Wako hunipa fahari, na inaonekana ya kuleta sifa kuu kwa mimi kuwa mmoja wa watu Wako. Nitatumia chochote na kutoa chochote ili kufanya mapenzi Yako, na nitayatoa maisha yangu yote, na juhudi za maisha yangu yote, Kwako.” Unapoomba hivi, kutakuwa na upendo usioisha na utiifu wa kweli kwa Mungu ndani ya moyo wako. Je, umewahi kuwa na tukio kama hili? Kama watu huguswa mara kwa mara na Roho wa Mungu, basi wako radhi hasa kujitolea wenyewe kwa Mungu katika maombi yao: “Ee Mungu! Ningependa kutazama siku Yako ya utukufu, na ningependa kuishi kwa ajili Yako—hakuna kilicho cha thamani au maana zaidi kuliko kuishi kwa ajili Yako, na sina hamu hata kidogo ya kuishi kwa ajili ya Shetani na mwili. Wewe huniinua kwa kuniwezesha mimi kuishi kwa ajili Yako leo.” Wakati ambapo umeomba kwa njia hii, utahisi kwamba huna budi ila kutoa moyo wako kwa Mungu, kwamba lazima umpate Mungu, na kwamba ungechukia kufa bila kumpata Mungu wakati ambapo uko hai. Baada ya kunena ombi hilo, kutakuwa na nguvu isiyoisha ndani yako, na hutajua hiyo hutoka wapi; ndani ya moyo wako kutakuwa na nguvu bila kikomo, na utakuwa na hisi kwamba Mungu ni wa kupendeza sana, na kwamba Anastahili kupendwa. Huu ndio wakati ambapo utakuwa umeguswa na Mungu. Wale wote ambao wamekuwa na tukio hilo wameguswa na Mungu. Kwa wale ambao mara kwa mara huguswa na Mungu, mabadiliko hutokea ndani ya maisha yao, wao huweza kufanya azimio lao na wako radhi kumpata Mungu kabisa, upendo kwa Mungu ndani yao ni thabiti zaidi, mioyo yao imeelekea kwa Mungu kabisa, wao huwa hawastahi familia, ulimwengu, matatizo, au siku zao za baadaye, na wao huwa radhi kutoa juhudi za maisha yote kwa Mungu. Wale wote ambao wameguswa na Roho wa Mungu ni watu wanaofuatilia ukweli, na ambao huwa na tumaini la kufanywa wakamilifu na Mungu.

Je, umeelekeza moyo wako kwa Mungu? Moyo wako umeguswa na Roho wa Mungu? Kama hujawahi kuwa na tukio kama hilo, na kama hujawahi kuomba kwa njia kama hiyo, basi hili linaonyesha kwamba Mungu hana nafasi ndani ya moyo wako. Wale wote ambao huongozwa na Roho wa Mungu na ambao wameguswa na Roho wa Mungu huwa na kazi ya Mungu, ambalo linaonyesha kwamba maneno ya Mungu na upendo wa Mungu vimekita mizizi ndani yao. Watu wengine husema: “Mimi si mwenye ari kama wewe katika maombi yangu, wala siguswi sana na Mungu: mara nyingine—wakati ambapo mimi hutafakari na kuomba—mimi huhisi kwamba Mungu ni wa kupendeza, na moyo wangu huguswa na Mungu.” Hakuna kilicho muhimu zaidi kuliko moyo wa mwanadamu. Wakati ambapo moyo wako umeelekea kwa Mungu, nafsi yako yote itakuwa imeelekea kwa Mungu, na wakati huo moyo wako utakuwa umeguswa na Roho wa Mungu. Wengi sana miongoni mwenu wamekuwa na tukio kama hilo—ni kwamba tu vina vya matukio yenu si sawa. Watu wengine husema: “Mimi huwa sisemi maneno mengi ya maombi, mimi husikiliza tu mawasiliano ya wengine na nguvu huongezeka

ndani yangu.” Hili huonyesha kwamba umeguswa na Mungu ndani. Watu ambao wameguswa na Mungu ndani hutiwa moyo wakati ambapo wao husikia mawasiliano ya wengine; kama moyo wa mtu hubaki bila kuathirika kabisa wanaposikia maneno ya kutia moyo, basi hili huthibitisha kwamba kazi ya Roho Mtakatifu haiko ndani yao. Hakuna shauku ndani yao, ambalo huthibitisha kwamba hawana azimio, na hivyo hawana kazi ya Roho Mtakatifu. Kama mtu ameguswa na Mungu, atakuwa na athari anaposikia maneno ya Mungu; kama hajaguswa na Mungu, basi hajajishughulisha na maneno ya Mungu, hayana uhusiano naye, na hana uwezo wa kupata nuru. Wale ambao wamesikia maneno ya Mungu na hawakuwa na athari ni watu ambao hawajaguswa na Mungu—ni watu ambao hawana kazi ya Roho Mtakatifu. Wale wote ambao wanaweza kukubali nuru mpya huguswa, na huwa na kazi ya Roho Mtakatifu.

Jitathmini mwenyewe:

1. Je, uko katikati ya kazi ya sasa ya Roho Mtakatifu?
2. Moyo wako umeelekea kwa Mungu? Umeguswa na Mungu?
3. Maneno ya Mungu yamekita mizizi ndani yako?
4. Je, utendaji wako umejengwa juu ya msingi wa masharti ya Mungu?
5. Wewe huishi chini ya uongozi wa nuru ya sasa ya Roho Mtakatifu?
6. Moyo wako hutawaliwa na dhana za zamani, au hutawaliwa na maneno ya Mungu leo?

Ukiyasikia maneno haya, athari iliyo ndani yenu ni gani? Baada ya kuamini kwa miaka hii yote, una maneno ya Mungu kama uzima wako? Je, kumekuwa na mabadiliko katika tabia yako potovu ya awali? Wewe, kwa mujibu wa maneno ya Mungu leo, unajua ni nini maana ya kuwa na uzima, na nini maana ya kutokuwa na uzima? Je, hili linaeleweka kwenu? Kilicho na umuhimu mkuu katika kumfuata Mungu ni kwamba kila kitu kinapaswa kuwa kwa kadri ya maneno ya Mungu leo: Kama unafuatilia kuingia katika uzima au kutimiza mapenzi ya Mungu, kila kitu kinapaswa kulenga maneno ya Mungu leo. Kama kile ambacho unawasiliana kwa karibu na kufuatilia hakilengi maneno ya Mungu leo, basi wewe ni mgeni kwa maneno ya Mungu, na umeondolewa kabisa katika kazi ya Roho Mtakatifu. Kile ambacho Mungu hutaka ni watu ambao huzifuata nyayo Zake. Haijalishi vile ulichoelewa awali ni cha ajabu na safi, Mungu hakitaki, na kama huwezi kuweka kando vitu hivyo, basi vitakuwa kizuizi kikubwa mno kwa kuingia kwako katika siku za baadaye. Wale wote ambao wanaweza kufuata nuru ya sasa ya Roho Mtakatifu wamebarikiwa. Watu wa enzi zilizopita pia walifuata nyayo za Mungu, ilhali hawangeweza kufuata mpaka leo; hii ndiyo baraka ya watu wa siku za mwisho. Wale ambao wanaweza kufuata kazi ya sasa ya Roho Mtakatifu, na ambao wanaweza kuzifuata nyayo za

Mungu, kiasi kwamba wamfuate Mungu popote Awaongozapo—hawa ni watu ambao wamebarikiwa na Mungu. Wale wasiofuata kazi ya sasa ya Roho Mtakatifu hawajaingia katika kazi ya maneno ya Mungu, na haijalishi wanafanya kazi kiasi gani, au mateso yao ni makubwa vipi, au wanakimbia hapa na pale kiasi gani, hakuna linalomaanisha chochote kwa Mungu kati ya hayo, na Yeye hatawasifu. Leo, wale wote ambao hufuata maneno ya sasa ya Mungu wako ndani ya mkondo wa Roho Mtakatifu; wale ambao ni wageni kwa maneno ya leo ya Mungu wako nje ya mkondo wa Roho Mtakatifu, na watu hao hawasifiwi na Mungu. Huduma ambayo imetenganishwa na matamshi ya sasa ya Roho Mtakatifu ni huduma ambayo ni ya mwili, na ya dhana, na haiwezi kuwa kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu. Kama watu huishi miongoni mwa dhana za kidini, basi hawawezi kufanya lolote lenye kustahili kwa mapenzi ya Mungu, na hata ingawa wao humhudumia Mungu, wao huhudumu katikati ya mawazo na dhana zao, na hawawezi kabisa kuhudumu kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu. Wale ambao hawawezi kuifuata kazi ya Roho Mtakatifu hawaelewi mapenzi ya Mungu, na wale ambao hawaelewi mapenzi ya Mungu hawawezi kumhudumia Mungu. Mungu hutaka huduma inayoupendeza moyo Wake mwenyewe; Hataki huduma ambayo ni ya dhana na mwili. Kama watu hawawezi kuzifuata hatua za kazi ya Roho Mtakatifu, basi wao huishi katikati ya dhana. Huduma ya watu hao hukatiza na huvuruga, na huduma ya aina hii huenda kinyume na Mungu. Hivyo wale ambao hawawezi kuzifuata nyayo za Mungu hawawezi kumhudumia Mungu; wale ambao hawawezi kuzifuata nyayo za Mungu humpinga Mungu bila shaka, na ni wasioweza kulingana na Mungu. “Kuifuata kazi ya Roho Mtakatifu” kuna maana ya kufahamu mapenzi ya Mungu leo, kuweza kutenda kwa mujibu wa masharti ya sasa ya Mungu, kuweza kutii na kumfuata Mungu wa leo, na kuingia kwa mujibu wa matamshi mapya zaidi ya Mungu. Huyu pekee ndiye mtu ambaye hufuata kazi ya Roho Mtakatifu na yuko ndani ya mkondo wa Roho Mtakatifu. Watu hao hawawezi tu kupokea sifa za Mungu na kumwona Mungu, lakini wanaweza pia kujua tabia ya Mungu kutoka kwa kazi ya karibuni zaidi ya Mungu, na wanaweza kujua dhana na ukaidi wa mwanadamu, na asili na kiini cha mwanadamu, kutoka kwa kazi Yake ya karibuni zaidi; pia, wanaweza kutimiza polepole mabadiliko katika tabia yao wakati wa huduma yao. Ni watu kama hawa pekee ndio wanaoweza kumpata Mungu, na ambao wamepata kwa halisi njia ya kweli. Wale ambao huondoshwa na kazi ya Roho Mtakatifu ni watu wasioweza kufuata kazi ya karibuni zaidi ya Mungu, na ambao huasi dhidi ya kazi ya karibuni zaidi ya Mungu. Kwamba watu hao humpinga Mungu waziwazi ni kwa sababu Mungu amefanya kazi mpya, na kwa sababu picha ya Mungu si sawa na ile iliyo ndani ya dhana zao—kutokana na hilo wao humpinga Mungu waziwazi na kumhukumu Mungu, kusababisha wao kuchukiwa na kukataliwa na Mungu. Kuwa na ufahamu wa kazi ya karibuni zaidi ya Mungu si jambo rahisi, lakini kama watu wana nia ya kutii kazi ya Mungu kwa kudhamiria na kuitafuta kazi ya Mungu, basi watakuwa na nafasi ya kumwona Mungu, na watakuwa na nafasi ya kupata uongozi mpya zaidi wa Roho Mtakatifu.

Wale ambao hupinga kazi ya Mungu kwa kudhamiria hawawezi kupata nuru ya Roho mtakatifu au uongozi wa Mungu. Hivyo, kama watu wanaweza kupokea kazi ya karibuni zaidi ya Mungu au la hutegemea neema ya Mungu, hutegemea ukimbizaji wao, na hutegemea makusudi yao.

Wale wote ambao huweza kutii matamshi ya sasa ya Roho Mtakatifu wamebarikiwa. Haijalishi vile walikuwa, au vile Roho Mtakatifu alikuwa akifanya kazi ndani yao—wale ambao wamepata kazi ya karibuni zaidi ni waliobarikiwa zaidi, na wale ambao hawawezi kufuata kazi ya karibuni zaidi huondoshwa. Mungu anataka wale wanaoweza kukubali nuru mpya, na Anataka wale ambao hukubali na kujua kazi Yake ya karibuni zaidi. Kwa nini husemwa kwamba lazima uwe mwanamwali safi? Mwanamwali safi anaweza kutafuta kazi ya Roho Mtakatifu na kuelewa mambo mapya, na zaidi ya hayo, kuweza kuweka kando dhana za zamani, na kutii kazi ya Mungu leo. Kundi hili la watu, ambao hukubali kazi mpya zaidi ya leo, walijaaliwa na Mungu kabla ya enzi, na ni ambao wamebarikiwa zaidi ya watu wote. Ninyi huisikia sauti ya Mungu moja kwa moja, na kutazama kuonekana kwa Mungu, na hivyo, kotekote mbinguni na duniani, na kotekote katika enzi, hakuna waliobarikiwa kuliko ninyi, hili kundi la watu. Haya yote ni kwa sababu ya kazi ya Mungu, kwa sababu ya majaaliwa na uteuzi wa Mungu, na kwa sababu ya neema ya Mungu; kama Mungu hangeongea na kutamka maneno Yake, hali zenu zingekuwa kama zilivyo leo? Vivi hivi, utukufu wote na sifa ziwe kwa Mungu, kwani haya yote ni kwa sababu Mungu huwainua ninyi. Na mambo haya yakiwa akilini, bado ungeweza kuwa baridi? Nguvu zako bado hazingeweza kuongezeka?

Kwamba wewe huweza kukubali hukumu, kuadibu, kuangamiza, na usafishaji wa maneno ya Mungu, na, aidha, unaweza kukubali maagizo ya Mungu, lilijaaliwa na Mungu mwanzoni mwa wakati, na hivyo lazima usihuzunishwe sana wakati ambapo wewe huadibiwa. Hakuna anayeweza kuondoa kazi ambayo imefanywa ndani yenu, na baraka ambazo zimetolewa ndani yenu, na hakuna anayeweza kuondoa yote ambayo mmepeva ninyi. Watu wa dini hawastahimili mlingano na ninyi. Ninyi hamna ubingwa mkuu katika Biblia, na hamjajizatiti na nadharia za kidini, lakini kwa sababu Mungu amefanya kazi ndani yenu, mmepata zaidi ya yeyote kotekote katika enzi—na kwa hiyo hii ni baraka yenu kuu zaidi. Kwa sababu ya hili, lazima mjitolee hata zaidi kwa Mungu, na hata waaminifu zaidi kwa Mungu. Kwa sababu Mungu hukuinua, lazima utegemeze juhudi zako, na lazima utayarishe kimo chako kukubali maagizo ya Mungu. Lazima usimame imara mahali ambapo Mungu amekupa, ufuatilie kuwa mmoja wa watu wa Mungu, ukubali mafunzo ya ufalme, upatwe na Mungu na hatimaye kuwa ushuhuda wa kuleta sifa kuu kwa Mungu. Je, wewe una maazimio haya? Kama una maazimio hayo, basi hatimaye una hakika ya kupatwa na Mungu, na utakuwa ushuhuda wa kuleta sifa kuu kwa Mungu. Unapaswa kuelewa kwamba agizo kuu ni kupatwa na Mungu na kugeuka kuwa ushuhuda wa kuleta sifa kuu kwa Mungu. Haya ni mapenzi ya Mungu.

Maneno ya Roho Mtakatifu leo ni nguvu za kazi ya Roho Mtakatifu, na kuendelea kwa Roho Mtakatifu kumpa nuru mwanadamu wakati wa kipindi hiki ni mwelekeo wa kazi ya Roho Mtakatifu. Na mwelekeo ni upi katika kazi ya Roho Mtakatifu leo? Ni uongozi wa watu ndani ya kazi ya Mungu leo, na ndani ya maisha ya kiroho ya kawaida. Kuna hatua kadhaa za kuingia katika maisha ya kiroho ya kawaida:

1. Kwanza, lazima uumimine moyo wako ndani ya maneno ya Mungu. Lazima usiyafuatilie maneno ya Mungu katika siku za zamani, na lazima usiyasome wala kuyafananisha na maneno ya sasa. Badala yake, lazima uumimine moyo wako kabisa katika maneno ya sasa ya Mungu. Kama kuna watu ambao bado wangependa kuyasoma maneno ya Mungu, vitabu vya kiroho, au maelezo mengine ya mahubiri kutoka kwa siku za zamani, ambao hawafuati maneno ya Roho Mtakatifu leo, basi wao ni wapumbavu zaidi ya watu wote; Mungu huchukia sana watu kama hao. Kama uko radhi kukubali nuru ya Roho Mtakatifu leo, basi mimina moyo wako kabisa katika matamshi ya Mungu leo. Hili ni jambo la kwanza ambalo lazima utimize.

2. Lazima uombe juu ya msingi wa maneno yaliyonenwa na Mungu leo, uingie ndani ya maneno ya Mungu na uwasiliane kwa karibu na Mungu, na ufanye maazimio yako mbele ya Mungu, ni viwango vipi ambavyo ungependa kufuatilia ufanikishaji wake.

3. Lazima ufuatilie kuingia kwa maana sana ndani ya ukweli juu ya msingi wa kazi ya Roho Mtakatifu leo. Usishikilie matamshi na nadharia zilizopitwa na wakati kutoka zamani.

4. Lazima utafute kuguswa na Roho Mtakatifu, na kuingia katika maneno ya Mungu.

5. Lazima ufuatilie kuingia katika njia ambayo Roho Mtakatifu anatembea leo.

Na ni vipi ambavyo wewe hutafuta kuguswa na Roho Mtakatifu? Kilicho muhimu ni kuishi ndani ya maneno ya sasa ya Mungu, na kuomba juu ya msingi wa masharti ya Mungu. Baada ya kuomba kwa njia hii, Roho Mtakatifu kwa kweli atakugusa. Kama hutafuti kwa kutegemea msingi wa maneno yaliyonenwa na Mungu leo, basi hili ni bure. Unapaswa kuomba, na kusema: “Ee Mungu! Mimi hukupinga Wewe, na unanidai Mimi mengi sana; mimi ni mkaidi sana, na siwezi kamwe kukuridhisha Wewe. Ee Mungu, natamani Wewe uniokoe, natamani kukupa Wewe huduma hadi mwisho kabisa, natamani kufa kwa ajili Yako. Wewe hunihukumu na kuniadibu, na sina malalamiko; mimi hukupinga Wewe na nastahili kufa, ili watu wote waweze kutazama tabia Yako yenye haki katika kifo changu.” Wakati ambapo wewe huomba kutoka moyoni mwako kwa njia hii, Mungu atakusikia, na atakuongoza; kama huombi juu ya msingi wa maneno ya Roho Mtakatifu leo, basi hakuna uwezekano wa Roho Mtakatifu kukugusa wewe. Kama wewe huomba kwa kadri ya mapenzi ya Mungu, na kwa kadri ya kile ambacho Mungu hutaka kufanya leo, utasema: “Ee Mungu! Nataka kukubali maagizo Yako na kuwa mwaminifu

kwa maagizo Yako, na niko radhi kuyatoa maisha yangu yote kwa utukufu Wako, ili yote nifanyayo yaweze kufikia kiwango cha watu wa Mungu. Moyo wangu na uweze kuguswa na Wewe. Nataka Roho Wako anipe nuru wakati wowote, kusababisha yote nifanyayo yalete aibu kwa Shetani, ili hatimaye nipatwe na Wewe.” Kama wewe huomba kwa njia hii, ukilenga mapenzi ya Mungu, basi Roho Mtakatifu atafanya kazi ndani yako bila kuzuilika. Haijalishi maneno ya maombi yako ni mangapi—kilicho muhimu ni kama unaelewa mapenzi ya Mungu au la. Huenda ninyi nyote mmekuwa na tukio lifuatalo: Wakati mwingine, ukiwa unaomba katika kusanyiko, nguvu za kazi ya Roho Mtakatifu hufikia kilele chake, kusababisha nguvu za kila mtu kuongezeka. Watu wengine hulika kwa uchungu na kutoa machozi huku wakiomba, kwa kulemewa na majuto mbele ya Mungu, na watu wengine huonyesha azimio lao, na kuweka nadhiri. Hiyo ndiyo athari ya kutimizwa na kazi ya Roho Mtakatifu. Leo, ni ya muhimu sana kwamba watu wote wamimine mioyo yao kabisa ndani ya maneno ya Mungu. Usisisitize kwa maneno yaliyonenwa awali; kama bado unashikilia kilichokuja awali, basi Roho Mtakatifu hatafanya kazi ndani yako. Je, waona vile hili ni muhimu?

Je, mnajua njia ambayo Roho Mtakatifu hutembea leo? Mawazo makuu kadhaa hapo juu ni kile kitakachotimizwa na Roho Mtakatifu leo na katika siku za baadaye; ni njia inayofuatwa na Roho Mtakatifu, na kuingia ambako kunapaswa kufuatiliwa na mwanadamu. Katika kuingia kwako maishani, kwa kiasi kidogo sana lazima umimine moyo wako ndani ya maneno ya Mungu, na uweze kukubali hukumu na kuadibu kwa maneno ya Mungu; moyo wako lazima uwe na shauku kwa Mungu, lazima ufuatilie kuingia kwa maana sana katika ukweli, na malengo ambayo Mungu hutaka. Wakati ambapo unakuwa na nguvu hizi, basi hilo huonyesha kuwa umeguswa na Mungu, na moyo wako umeanza kuelekea kwa Mungu.

Hatua ya kwanza ya kuingia katika uzima ni kuumimina moyo wako kabisa ndani ya maneno ya Mungu, na hatua ya pili ni kukubali kuguswa na Roho Mtakatifu. Ni nini athari ya kutimizwa kwa kukubali kuguswa na Roho Mtakatifu? Kuweza kuwa na shauku ya, kutafuta, na kuchunguza ukweli wa maana sana, na kuwa na uwezo wa kushirikiana na Mungu katika njia nzuri. Leo, wewe hushirikiana na Mungu, ambalo ni kusema kuna lengo kwa ukimbizaji wako, kwa maombi yako, na kwa mawasiliano yako ya maneno ya Mungu, na wewe hutekeleza wajibu wako kwa mujibu wa masharti ya Mungu—huku pekee ndiko kushirikiana na Mungu. Ukizungumza tu kuhusu kumwacha Mungu atende, lakini usichukue hatua yoyote, wala kuomba au kutafuta, basi hili lingeweza kuitwa ushirikiano? Kama huna chochote kuhusu ushirikiano ndani yako, na umeondolewa mafunzo ya kuingia ambayo yana lengo, basi wewe hushirikiani? Watu wengine husema: “Kila kitu hutegemea majaaliwa ya Mungu, yote hufanywa na Mungu mwenyewe: kama Mungu hangelifanya, basi mwanadamu angewezaje?” Kazi ya Mungu ni ya kawaida, na siyo ya rohoni hata kidogo, na ni kupitia tu kwa utafutaji wako wa utendaji ndiyo

Roho Mtakatifu hufanya kazi, kwani Mungu hamlazimishi mwanadamu—lazima umpe Mungu nafasi ya kufanya kazi, na kama hufuatilii au kuingia, na kama hakuna shauku hata kidogo ndani ya moyo wako, basi Mungu hana nafasi ya kufanya kazi. Ni kwa njia ipi ndio unaweza kutafuta kuguswa na Mungu? Kupitia maombi, na kuja karibu na Mungu. Lakini la muhimu zaidi, kumbuka, lazima iwe juu ya msingi wa maneno yanayonenwa na Mungu. Wakati ambapo unaguswa mara kwa mara na Mungu, hutawaliwi kabisa na mwili: Mume, mke, watoto, na pesa—yote ni yasiyoweza kukufunga wewe, na wewe hutamani kufuatilia tu ukweli na kuishi mbele ya Mungu. Wakati huu, utakuwa mtu anayeishi katika eneo la uhuru.

Wale Ambao Tabia Zao Imebadilika ni Wale Ambao Wameingia Katika Uhalisi wa Neno la Mungu

Njia ambayo Roho Mtakatifu huchukua ndani ya watu ni kuvuta kwanza mioyo yao kutoka kwa watu, matukio, na vitu vyote, na kuingiza ndani ya maneno ya Mungu ili ndani ya mioyo yao wote waamini kwamba maneno ya Mungu hayana shaka kabisa na ni kweli kabisa. Kwa vile unaamini katika Mungu lazima uamini katika maneno Yake; ikiwa umeamini katika Mungu kwa miaka mingi lakini hujui njia ambayo Roho Mtakatifu hufuata, wewe kweli ni muumini? Ili kutimiza maisha ya mtu wa kawaida na maisha yanayofaa ya mtu na Mungu, lazima kwanza uamini maneno Yake. Ikiwa hujakamilisha hatua ya kwanza ya kazi ambayo Roho Mtakatifu hufanya ndani ya watu, huna msingi. Unakosa kanuni ya msingi kabisa, kwa hiyo unawezaje kutembea njia iliyo mbele? Kufuata njia sahihi ya Mungu kumkamilisha mwanadamu ni kuingia katika njia sahihi ya kazi halisi ya Roho Mtakatifu; pia ni kufuata njia ambayo Roho Mtakatifu hutembea. Hivi sasa, njia ambayo Roho Mtakatifu hutembea ni maneno halisi ya Mungu. Kwa hiyo, kwa mtu kuitembea, ni lazima atii, na kula na kunywa maneno halisi ya Mungu mwenye mwili. Anafanya kazi ya neno, na kila kitu kinaanza kutoka kwa neno Lake, na kila kitu kinaanzishwa juu ya neno Lake, neno Lake la sasa. Kama ni kuwa bila shaka yoyote kabisa kuhusu Mungu kuwa mwili au kumjua Yeye, mtu anapaswa kuweka bidii zaidi katika maneno Yake. Vinginevyo, hawezi kutimiza chochote kamwe, na ataachwa bila chochote. Ni kwa kuja kumjua Mungu tu na kumridhisha kwa msingi wa kula na kunywa maneno Yake ndipo mtu anaweza kuanzisha polepole uhusiano unaofaa na Yeye. Kula na kunywa maneno Yake na kuyaweka katika matendo ni ushirikiano bora zaidi na Mungu, na ni kitendo kinachotoa ushuhuda vizuri zaidi kama mmoja wa watu Wake. Mtu akielewa na aweze kutii kiini cha maneno halisi ya Mungu, anaishi katika njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu na ameingia katika njia sahihi ya Mungu kumkamilisha mwanadamu. Zamani ilikuwa kwamba watu walitafuta neema na walitafuta amani na furaha, na kisha waliweza kupata kazi ya Mungu. Ni tofauti sasa. Ikiwa hawana maneno ya Mungu aliyepata mwili, ikiwa hawana uhalisi wa maneno

hayo, hawawezi kupata kibali kutoka kwa Mungu na wataondoshwa na Mungu. Ili kutimiza maisha ya kiroho ya kufaa, kwanza kula na kunywa maneno ya Mungu na kuyaweka katika vitendo; na juu ya msingi huu anzisha uhusiano wa kufaa kati ya mwanadamu na Mungu. Ni vipi ambavyo unashirikiana? Ni vipi ambavyo unakuwa shahidi kama mmoja wa watu Wake? Ni vipi ambavyo unaanzisha uhusiano wa kufaa na Mungu?

Hivi ndivyo namna ya kuona ikiwa una uhusiano wa kufaa na Mungu katika maisha yako ya kila siku:

1. Unaamini ushuhuda wa Mungu mwenyewe?
2. Unaamini katika moyo wako kwamba maneno ya Mungu ni kweli na yasiyoweza kukosea?
3. Wewe ni mtu unayeweka maneno Yake katika vitendo?
4. Umejitolea kwa kile Alichokuaminia? Unawezaje kujitolea kwa hicho?
5. Je, kila kitu unachofanya ni kwa ajili ya kumridhisha na kuwa mwaminifu kwa Mungu?

Kupitia mambo haya, unaweza kutathmini ikiwa una uhusiano wa kufaa na Mungu katika hatua hii ya sasa.

Ikiwa unaweza kukubali kile Mungu anakuaminia wewe, kukubali ahadi Yake, na kufuata njia ya Roho Mtakatifu, hii ni kufanya mapenzi ya Mungu. Una uwazi wa ndani kuhusu njia ya Roho Mtakatifu? Je, matendo yako ya sasa ni ya kufuatana na njia Yake? Moyo wako unasonga karibu na Mungu? Uko radhi kuifuata nuru mpya kabisa kutoka kwa Roho Mtakatifu? Uko radhi kupatwa na Mungu? Uko radhi kuwa dhihirisho la utukufu wa Mungu duniani? Una nia ya kutimiza anachohitaji Mungu? Ikiwa, mara tu Mungu anapozungumza, na una azimio la kushirikiana na Yeye na kumridhisha Yeye, ikiwa hii ndiyo hali ya saikolojia yako ya ndani, inamaanisha kwamba maneno ya Mungu yamezaa matunda ndani ya moyo wako. Ikiwa huna aina hiyo ya hiari na huna lengo katika kazi yako, inamaanisha kwamba moyo wako bado haujasisimuliwa na Mungu.

Kwa vile watu wameingia rasmi katika mafundisho ya ufalme, masharti ya Mungu kwao yameinuliwa. Mtu anawezaje kuona hilo? Ilisemekana awali kwamba watu hawana uzima, lakini sasa watu wanatafuta uzima, wanatafuta kuwa mmoja wa watu wa Mungu, na kupatwa na kukamilishwa na Mungu. Je, huku sio kuinuliwa? Kwa kweli, masharti kwa watu ni rahisi kuliko yalivyokuwa. Watu hawahitajiki kuwa watendaji huduma au kufa—wanayotakiwa tu ni kuwa watu wa Mungu. Je, hilo si rahisi zaidi? Bora tu uutoe moyo wako kwa Mungu na kutii uongozi

Wake, yote yatafaulu. Mbona unadhani ni vigumu sana? Kile kinachozungumziwa sasa kuhusu kuingia katika uzima ni dhahiri zaidi kuliko hapo awali; watu hawakuwa na udhahiri na hawakujua uhalisi wa uzima unahusu nini. Wale walio na athari kwa kusikia maneno ya Mungu, walio na nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu, na ambao wamepata kukamilishwa Kwake na mabadiliko katika tabia mbele Yake—watu hawa wote wana uzima. Kila ambacho Mungu anataka ni viumbe wenye uhai, sio vitu visivyo na uhai. Ikiwa huna uhai, huna uzima, na Mungu hatanena nawe, na hasa Hatakuinua kuwa mmoja wa watu Wake. Kwa vile mmeinuliwa na Mungu, kwa vile mmepokea baraka kubwa kama hii kutoka Kwake, hii inamaanisha kwamba nyinyi nyote ni watu walio na uzima, na wale walio na uzima hutoka kwa Mungu.

Ili mtu kufuatilia mabadiliko katika tabia ya maisha yake, njia ya kutenda ni rahisi. Ikiwa unaweza kufuata maneno halisi ya Roho Mtakatifu katika uzoefu wako wa utendaji, utaweza kutimiza mabadiliko katika tabia yako. Ikiwa utafuata na kutafuta chochote ambacho Roho Mtakatifu husema, wewe ni mtu anayemtii Yeye, na kwa njia hii utaweza kuwa na mabadiliko katika tabia. Tabia ya mwanadamu hubadilika na maneno halisi ya Roho Mtakatifu; ikiwa kila mara wewe hutetea uzoefu wako wa zamani na sheria, tabia yako haitabadilika. Ikiwa Roho Mtakatifu angezungumza leo kuwaambia watu wote waingie katika uzima wa ubinadamu wa kawaida lakini ukaendelea kulenga sehemu ya juu na kuchanganyikiwa kuhusu uhalisi na usiuchukulie kwa makini, utakuwa mtu ambaye haendelei na kazi Yake na hutakuwa mtu aliyeingia katika njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu. Ikiwa tabia yako inaweza kubadilika au la inategemea na ikiwa unaweza kuendelea na maneno halisi ya Roho Mtakatifu au la na una ufahamu wa kweli. Hili ni tofauti na kile mlichoelewa awali. Kile ulichoelewa kuhusu mabadiliko katika tabia awali kilikuwa kwamba wewe, ambaye ni rahisi kuhukumu, kupitia kwa kufundishwa nidhamu na Mungu huzungumzi ovyo ovyo tena. Lakini hii ni hali moja tu ya mabadiliko, na hivi sasa suala muhimu zaidi ni kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu. Unafuata chochote asemacho Mungu; unatii chochote asemacho Yeye. Watu hawawezi kubadilisha tabia yao wenyewe; lazima wapitie hukumu na kuadibu, mateso na usafishaji wa maneno ya Mungu, au kushughulikiwa, kufunzwa nidhamu, na kupogolewa na maneno Yake. Ni baada ya hapo tu ndipo wanaweza kutimiza utiifu na ibada kwa Mungu, na wasijaribu tena kumdanganya Yeye na kumshughulikia kwa uzembe. Ni kupitia kwa usafishaji wa maneno ya Mungu ndio watu hupata mabadiliko katika tabia. Ni wale tu wanaopitia mfichuo, hukumu, kufundishwa nidhamu, na kushughulikiwa kwa maneno Yake ambao hawatathubutu tena kufanya mambo kwa kutojali, na watakuwa watulivu na makini. Jambo muhimu sana ni kwamba wanaweza kutii neno la sasa la Mungu na kutii kazi ya Mungu, na hata kama hayalingani na fikira za binadamu, wanaweza kuweka kando fikira hizi na kutii kwa hiari. Mabadiliko katika tabia yalipozungumziwa hapo awali, imekuwa hasa kuhusu kujinyima mwenyewe, kuruhusu mwili kuteseka, kufunza nidhamu

mwili wa mtu, na kujiondolea mapendeleo ya mwili—hii ni aina moja ya mabadiliko katika tabia. Watu sasa wanajua kwamba maonyesho halisi ya mabadiliko katika tabia ni kutii maneno halisi ya Mungu na vilevile kuweza kuwa na ufahamu halisi wa kazi Yake mpya. Kwa njia hii, ufahamu wa awali wa watu kumhusu Mungu, ambao ulipotoshwa na fikira zao wenyewe, na kutimiza ufahamu wa kweli wa na utiifu Kwake. Hii tu ndio maonyesho halisi ya mabadiliko katika tabia.

Kufuatilia kwa watu kuingia katika uzima kunalingana na maneno ya Mungu; imesemwa hapo awali kwamba kila kitu hutimizwa kwa sababu ya maneno Yake, lakini hakuna aliyeona ukweli. Ikiwa katika hatua hii utaingia katika uzoefu utakuwa wazi kabisa—huku ni kujenga msingi mzuri kwa majaribio ya siku za baadaye, na haijalishi anachosema Mungu, unatakiwa tu kuingia katika maneno Yake. Mungu anaposema Anaanza kuadibu watu, unakubali kuadibu Kwake. Mungu anapowauliza watu wafe, unakubali jaribio hilo. Ikiwa kila mara unaishi ndani ya matamshi Yake mapya zaidi, mwishowe maneno ya Mungu yatakukamilisha wewe. Kadri unavyoingia katika maneno ya Mungu, ndivyo utakavyokamilisha haraka zaidi. Kwa nini Ninawasiliana tena na tena na kuwaambia muelewe na kuingia katika maneno ya Mungu? Ni kwa kulenga tu kazi yako kwa maneno ya Mungu na kuyapitia na kuingia katika uhalisi wake ndipo Roho Mtakatifu atakuwa na nafasi ya kufanya kazi ndani yako. Kwa hiyo nyote ni washindani katika kila mbinu ya kazi ya Mungu, na haijalishi ikiwa mateso yenu yamekuwa makubwa au madogo mwishowe, nyote mtapata “hidaya”. Ili kutimiza ukamilifu wenu wa mwisho, lazima muingie katika maneno yote ya Mungu. Kwa Roho Mtakatifu kuwakamilisha watu, Hafanyi kazi kwa upande mmoja tu. Anahitaji ushirikiano wa watu; Anahitaji kila mtu ashirikiane Naye kwa makusudi. Haijalishi anachosema Mungu, unaingia tu katika maneno Yake—hii ni ya manufaa zaidi kwa maisha yenu. Kila kitu ni kwa ajili ya mabadiliko yenu katika tabia. Unapoingia katika maneno ya Mungu, moyo wako utasisimuliwa na Mungu, na utaweza kuelewa kila kitu ambacho Mungu anataka kutimiza katika hatua hii ya kazi, na utakuwa na nia ya kukitimiza. Katika wakati wa kuadibu, baadhi ya watu waliamini kwamba hiyo ilikuwa mbinu ya kazi na hawakuamini katika maneno ya Mungu. Kutokana na hilo, hawakupitia usafishaji na wakatoka katika wakati wa kuadibu bila kupata chochote na hawakuelewa chochote. Kuna baadhi ambao huingia kwa hakika katika maneno haya bila chembe ya shaka yoyote; wanasema kuwa maneno ya Mungu ni kweli na yasioweza kukosea na kwamba watu wanapaswa kuadibiwa. Wanang’ang’ana katika hili kwa kipindi fulani cha wakati na kuachilia siku zao za baadaye na majaliwa yao, na wanapotoka tu hapo tabia yao huwa imebadilika vilivyo na wao huwa na hata ufahamu wa kina zaidi kuhusu Mungu. Wale ambao wametoka katikati ya kuadibu wote huhisi kupendeza kwa Mungu, na wanajua kwamba hatua hiyo ya kazi ya Mungu ni upendo Wake mkuu ukija juu ya wanadamu, kwamba ni ushindi na

wokovu wa upendo wa Mungu. Nao pia husema kwamba mawazo ya Mungu ni mazuri kila mara, na kila jambo ambalo Mungu hufanya ndani ya mwanadamu ni upendo, sio chuki. Wale wasioamini maneno ya Mungu au kuyachukulia kuwa muhimu hawakupitia usafishaji katika wakati wa kuadibu, na matokeo yake ni kwamba Roho Mtakatifu haandamani nao, na hawajapata chochote. Kwa wale walioingia katika wakati wa kuadibu, ingawa walipitia usafishaji, Roho Mtakatifu alikuwa anafanya kazi ndani yao kwa njia iliyofichika, na matokeo ni kwamba walipitia mabadiliko katika tabia yao ya maisha. Watu wengine huonekana kuwa wazuri sana kwa nje. Kila mara wao huwa na furaha, lakini hawajaingia katika hali hiyo ya usafishaji wa maneno ya Mungu na hawajabadilika kamwe, ambayo ni matokeo ya kutoamini maneno ya Mungu. Ikiwa huamini maneno Yake Roho Mtakatifu hatafanya kazi ndani yako. Mungu huonekana kwa wote wanaoamini maneno Yake; wale wanaoamini na kufahamu maneno Yake watakata upendo Wake!

Ili kuingia katika uhalisi wa maneno ya Mungu, unapaswa kupata njia ya kutenda na ujue jinsi ya kuweka maneno ya Mungu katika vitendo. Ni hivi tu ndivyo kutakuwa na mabadiliko katika tabia ya maisha yako, ni kwa njia hii tu ndiyo utaweza kukamilishwa na Mungu, na watu tu ambao wamekamilishwa na Mungu kwa njia hiyo ambao wanaweza kuwa sambamba na mapenzi Yake. Kupokea nuru mpya, lazima uishi ndani ya maneno Yake. Ikiwa umesisimuliwa na Roho Mtakatifu mara moja pekee, hiyo haitoshi kamwe—lazima uzame ndani zaidi. Wale ambao wamesisimuliwa mara moja pekee ari iliyo ndani yao imeamshwa hivi karibuni na wanakuwa radhi kutafuta, lakini hawawezi kudumisha hilo kwa kipindi kirefu, na lazima wapokee kila mara kuisimuliwa na Roho Mtakatifu. Kuna nyakati nyingi Nimetaja kuwa Natarajia kwamba Roho wa Mungu aweze kuisimua roho za watu, kwamba wafuatilie mabadiliko katika tabia ya maisha yao, na wanapotafuta kuisimuliwa na Mungu wafahamu udhaifu wao, na kwamba wakati wa kupitia maneno Yake, waondoe mambo machafu ndani yao (kujidai, kiburi, na fikira zao wenyewe, na kadhalika.) Usiamini kwamba kupokea tu kwa utendaji nuru mpya kunafaa—lazima pia uachane na vitu kutoka kwa hali mbaya. Hamhitaji tu kuingia kutoka kwa hali nzuri, lakini pia mnahitaji kujisafisha wenyewe kutoka kwa mambo yote machafu katika hali mbaya. Lazima ujichunguze siku zote na uone ni mambo yapi machafu bado yako ndani yako. Fikira za watu za kidini, makusudi, matarajio, kujidai, na kiburi yote ni mambo machafu. Jilinganishe na maneno yote ya Mungu ya ufunuo, na ujangalie ndani yako kuona fikira zozote za kidini unazoshikilia, Ukizitambua kwa kweli tu ndipo unaweza kuziacha. Baadhi ya watu husema: “Inatosha sasa kufuata tu nuru ya kazi ya wakati huu ya Roho Mtakatifu bila kushughulika kuhusu kitu kingine chochote.” Basi ni vipi ambavyo utaondoa fikira zako za kidini zinapojitokeza? Unadhani ni rahisi hivyo kufuata maneno ya Mungu? Ndani ya maisha yako halisi, bado kuna mambo ya kidini yanayoweza kuwa ya kuvuruga, na mambo haya

yanapojitokeza, yanaweza kuvuruga uwezo wako wa kukubali mambo mapya. Haya yote ni matatizo ambayo huwepo kwa kweli. Ikiwa utafuatilia tu maneno halisi ya Roho Mtakatifu huwezi kuridhisha mapenzi ya Mungu. Unapofuatilia nuru ya sasa ya Roho Mtakatifu, unapaswa kutambua ni fikira na makusudi gani ambayo bado unashikilia, ni kujidai gani kwa binadamu kupo hasa, na ni mienendo gani inakosa kumtii Mungu. Na baada ya kutambua mambo haya yote, lazima uachane nayo. Kukufanya wewe utupe matendo na mienendo yako ya awali yote ni kwa ajili ya kuyafuata maneno ya sasa ya Roho Mtakatifu. Kwa mabadiliko katika tabia, kwa upande mmoja, yanatimizwa kupitia kwa maneno ya Mungu, na kwa upande mwingine, yanahitaji watu washirikiane. Yaani, kazi ya Mungu na kutenda kwa watu vyote ni vya lazima.

Katika njia yako ya baadaye ya huduma, unawezaje kutimiza mapenzi ya Mungu? Jambo moja muhimu ni kufuatilia kuingia katika uzima, kufuatilia mabadiliko katika tabia, na kufuatilia kuingia kwa kina zaidi ndani ya ukweli—hii ndiyo njia ya kutimiza kufanywa mkamilifu na kupatwa na Mungu. Nyote mnapaswa kupokea agizo la Mungu, kwa hiyo ni nini hicho? Hii inahusiana na hatua inayofuata ya kazi, ambayo itakuwa kazi kuu zaidi itakayotekelezwa kotekote katika ulimwengu mzima. Kwa hiyo sasa mnapaswa kufuatilia mabadiliko katika tabia yenu ya maisha ili muwe kweli thibitisho la Mungu kupata utukufu kupitia kwa kazi Yake katika siku za baadaye, na kufanywa kuwa vielelezo vya kazi Yake ya siku za baadaye. Kazi yote ya leo inaweka msingi kwa ajili ya kazi ya siku za baadaye; ni kwa wewe kutumiwa na Mungu na ili uweze kuwa na ushuhuda Wake. Ikiwa hii ni chombo cha kazi yako, utaweza kupata uwepo wa Roho Mtakatifu. Kadri chombo cha kazi yako kilivyo juu, ndivyo itawezekana kwako wewe kukamilishwa zaidi. Kadri unavyofuatilia ukweli, ndivyo Roho Mtakatifu atafanya kazi zaidi. Kadri unavyokuwa na nguvu zaidi kwa kazi, ndivyo utakavyopata zaidi. Roho Mtakatifu huwakamilisha watu kulingana na hali yao ya ndani. Baadhi ya watu husema kwamba hawako radhi kutumiwa na Mungu au kukamilishwa na Yeye, kwamba itakuwa sawa alimuradi mwili wao unabaki salama na kamili na hawapitii msiba wowote. Watu wengine hawako radhi kuingia katika ufalme, lakini wako radhi kushuka katika shimo lisilo na mwisho. Katika hali hiyo, Mungu atakupa matamano hayo. Chochote unachofuatilia, Mungu atakutimizia. Kwa hiyo unafuatilia nini sasa? Je, unafuatilia kukamilishwa? Matendo na mienendo yako ya sasa ni kwa ajili ya kufanywa mkamilifu na Mungu, kwa ajili ya kupatwa na Yeye? Ni lazima siku zote ukipime kwa njia hii katika maisha yako ya kila siku. Ukilenga moyo wako katika kufuatilia lengo moja, Mungu bila shaka atakukamilisha. Hii ni njia ya Roho Mtakatifu. Njia inayoongozwa na Roho Mtakatifu inapatikana kupitia kwa kutafuta kwa watu. Kadri unavyotamani kukamilishwa na kupatwa na Mungu, ndivyo Roho Mtakatifu atafanya kazi zaidi ndani yako. Kadri usivyotafuta, na kadri unavyokuwa mbaya na kukimbia, ndivyo zaidi Roho Mtakatifu anakosa nafasi za kufanya kazi. Roho Mtakatifu atakuacha polepole. Uko radhi

kukamilishwa na Mungu? Uko radhi kupatwa na Mungu? Uko radhi kutumiwa na Mungu? Mnapaswa kufuatilia kufanya kila kitu kwa ajili ya kukamilishwa, kupatwa, na kutumiwa na Mungu, kuruhusu kila kitu katika ulimwengu kuona matendo ya Mungu yakifichuliwa ndani yenu. Miongoni mwa mambo yote, nyinyi ni watawala wa hayo, na miongoni mwa yote yaliyopo, mtamruhusu Mungu kupata ushuhuda Wake na utukufu Wake kwa sababu yenu—hii inaonyesha kwamba nyinyi ni kizazi kilichobarikiwa zaidi.

Kuhusu Kuutuliza Moyo Wako Mbele ya Mungu

Kuutuliza moyo wako mbele ya Mungu ni mojawapo ya hatua muhimu sana za kuingia katika maneno ya Mungu, na ni funzo ambalo watu wote sasa wana haja ya haraka kuingia ndani. Njia za kuingia za kuutuliza moyo wako mbele ya Mungu ni:

1. Ondoa moyo wako kwa mambo ya nje, tulia mbele ya Mungu, na uombe Mungu kwa moyo uliolenga.
2. Moyo wako ukiwa umetulia mbele ya Mungu, kula, kunywa, na kufurahia maneno ya Mungu.
3. Tafakari na uzingatie maneno ya Mungu na kufikiria kazi ya Mungu kwa moyo wako.

Kwanza anza na jambo la sala. Kuwa na nia moja, na uombe wakati usiobadilika. Haijalishi umepungukiwa na muda namna gani, au uwe na shughuli vipi, au chochote kitakachokufanyikia, omba kila siku kama kawaida, na ule na kunywa maneno ya Mungu kama kawaida. Mradi unakula na kunywa maneno ya Mungu, haijalishi mazingira yako ni yapi, utakuwa na raha nyingi katika roho yako, na hutasumbuliwa na watu, matukio, au mambo yanayokuzunguka. Unapotafakari juu ya Mungu kwa kawaida ndani ya moyo wako, kinachoendelea nje hakiwezi kukusumbua wewe. Hii ndiyo maana ya kuwa na kimo. Anzia kwa maombi: Kuomba kwa amani mbele ya Mungu huzaa matunda zaidi. Baada ya hapo, kuna kula na kunywa maneno ya Mungu, kuweza kuelewa mwangaza ulio kwenye maneno ya Mungu, kuweza kupata njia ya kutenda, kujua maazimio ya matamshi ya Mungu ni yapi, na kuelewa bila mkengeuko. Kwa kawaida, lazima moyo wako uweze kusongea karibu na Mungu kwa kawaida, lazima uweze kuzingatia upendo wa Mungu, kutafakari juu ya maneno ya Mungu, na usiweze kuathiriwa na kuingiliwa kwa dunia ya nje. Moyo wako unapokuwa na amani mbele ya Mungu kiasi kwamba unaweza kutafakari, ukiwa, ndani yako mwenyewe, unazingatia upendo wa Mungu, na kusonga karibu na Mungu kwa kweli, bila kujali mazingira uliyomo, na, kwa hakika ukiwa umefika kiwango ambacho unapeana sifa moyoni mwako, na ni bora zaidi hata kuliko kuomba, basi katika hili utakuwa wa kimo fulani. Ikiwa una uwezo wa kutimiza hali iliyoelezewa hapa juu, basi hii itathibitisha kuwa moyo wako kwa kweli uko na amani mbele ya Mungu. Hii ni hatua ya

kwanza; ni ujuzi wa kimsingi. Ni baada tu ya kuwa na uwezo wa kuwa na amani mbele ya Mungu ndipo watu wanaweza kuguswa na Roho Mtakatifu, na kupata nuru na kuangaziwa na Roho Mtakatifu, ni hapo tu ndipo wanaweza kuwasiliana kwa karibu kwa kweli na Mungu, na kuweza kushika mapenzi ya Mungu na mwongozo wa Roho Mtakatifu—na katika hii, watakuwa wameingia katika njia sahihi katika maisha yao ya kiroho. Kujizoeza mwenyewe kuishi mbele ya Mungu kufikia kina fulani ili uweze kujiasi mwenyewe, kujidharau mwenyewe, na kuishi katika maneno ya Mungu, hii kweli ni kuutuliza moyo wako mbele ya Mungu. Kuweza kujidharau, kujilaani, na kujiasi ni matokeo ambayo kazi ya Mungu hutimiza, na watu hawawezi kufanya hili. Kwa hivyo mazoezi ya kuutuliza moyo wa mtu mbele ya Mungu ni funzo ambalo watu wanapaswa kuingia ndani mara moja. Watu wengine hawawezi tu kwa kawaida kuituliza mioyo yao mbele ya Mungu, lakini mioyo yao hata haitulii mbele ya Mungu wanapoomba. Hii kwa jumla ni mbali sana na viwango vya Mungu! Ikiwa moyo wako hauwezi kutulia mbele ya Mungu unaweza kulisimuliwa na Roho Mtakatifu? Ikiwa huwezi kutulia mbele ya Mungu, unaweza kuvurugwa mawazo mtu akija, unaweza kuvurugwa mawazo watu wanapooonea, na moyo wako unaweza kuvutwa mbali watu wengine wanapofanya mambo, kwa hiyo wewe si mtu anayeishi mbele ya Mungu. Ikiwa moyo wako kweli umetulia mbele ya Mungu hutasumbuliwa na chochote kinachoendelea huko nje duniani, na hakuna mtu, tukio au jambo litakalokumiliki. Ikiwa mmeingia katika hili, basi zile hali hasi na mambo yote hasi—fikira za binadamu, falsafa za kuishi, mahusiano yasiyo ya kawaida na watu, na mawazo ndani ya moyo wako yatatoweka kwa kawaida. Kwa sababu kila mara unatafakari maneno ya Mungu, na moyo wako kila mara unasonga karibu na Mungu na kumilikiwa na maneno ya sasa ya Mungu, mambo hayo mabaya huvuliwa bila kufahamu. Mambo mapya mazuri yanapokumiliki, mambo ya zamani mabaya hayatakuwa na nafasi, kwa hiyo usitilie maanani mambo hayo mabaya. Huhitaji kufanya jitihada za kujaribu kuyadhibiti. Tilia maanani kutulia mbele ya Mungu, kula na kunywa maneno zaidi ya Mungu na kuyafurahia, imba nyimbo nyingi zaidi za dini ukimsifu Mungu, na wacha Mungu awe na nafasi ya kukushughulikia, kwa sababu Mungu wakati huu anataka binafsi kuwakamilisha watu, Anataka kuupata moyo wako, Roho Wake husisimua moyo wako, na ukiishi mbele ya Mungu ukifuata uongozi wa Roho Mtakatifu utamridhisha Mungu. Ukitilia maanani kuishi katika maneno ya Mungu na kushiriki zaidi kuhusu ukweli ili kupata nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu, basi fikira hizo za kidini, kujidai na kujikweza vitatoweka vyote, na kisha utajua namna ya kugharimia rasilmali kwa ajili ya Mungu, kujua namna ya kumpenda Mungu, na namna ya kumridhisha Mungu. Mambo hayo nje ya Mungu kisha husahaulika bila kufahamu.

Kutafakari juu ya maneno ya Mungu na kusali juu ya maneno ya Mungu kwa wakati sawa na kula na kunywa maneno ya sasa ya Mungu—hii ndiyo hatua ya kwanza ya kuwa na amani

mbele ya Mungu. Iwapo unaweza kuwa na amani kwa uhakika mbele ya Mungu, basi utafuatwa na nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu. Maisha yote ya kiroho hutimizwa kwa kutegemea kutulia mbele ya Mungu. Katika kuomba lazima utulie mbele ya Mungu kabla ya kuweza kulisimuliwa na Roho Mtakatifu. Kwa kutulia mbele ya Mungu unapokula na kunywa maneno ya Mungu unaweza kupata nuru na kuangaziwa na kuweza kutimiza kwa kweli ufahamu wa maneno ya Mungu. Katika tafakuri na ushirika wako wa kawaida, na wakati unasonga karibu na Mungu na moyo wako, ni wakati unapotulia tu mbele ya Mungu ndipo unaweza kuwa na ukaribiano halisi na Mungu, ufahamu halisi wa upendo wa Mungu na kazi ya Mungu, na uangalifu wa kweli kwa makusudi ya Mungu. Kadri unavyoweza kwa kawaida kutulia mbele ya Mungu ndivyo unavyoweza kuangaziwa zaidi, na ndivyo unavyoweza kufahamu tabia yako mwenyewe ya upotovu zaidi, unachokosa, unachopaswa kuingia, shughuli unayopaswa kuhudumu, na pale ulipo na dosari. Haya yote hutimizwa kwa kutegemea kuwa mtulivu mbele ya Mungu. Ikiwa utafikia kweli kina fulani cha kuwa mtulivu mbele ya Mungu, unaweza kugusa miujiza fulani katika roho, kugusa kile ambacho Mungu wakati huu anataka kufanya juu yako, kugusa ufahamu wa kina wa maneno ya Mungu, na kugusa asili ya maneno ya Mungu, kiini cha maneno ya Mungu, nafsi ya maneno ya Mungu, na unaweza kuona njia ya kutenda kwa kweli zaidi na sawasawa zaidi. Ikiwa huwezi kutulia katika roho yako kwa kina fulani, utaweza kulisimuliwa tu kiasi na Roho Mtakatifu, ndani utahisi nguvu, na furaha na amani kiasi, lakini hutagusa chochote kwa kina zaidi. Nimesema hapo awali, ikiwa mtu hatumii nguvu zake zote, itakuwa vigumu kwake kusikia sauti Yangu au kuona uso Wangu. Hii inanena juu ya kutimiza kina katika kutulia mbele ya Mungu, sio kwa juhudi za nje. Mtu anayeweza kuwa mtulivu kwa kweli mbele ya Mungu anaweza kujiachilia huru kutoka kwa vifungo vyote vya kidunia na anaweza kutimiza kumilikiwa na Mungu. Watu wote wasioweza kutulia mbele ya Mungu ni wafisadi na wasiozuiwa kwa yakini. Wale wote wanaoweza kutulia mbele ya Mungu ni watu ambao ni wacha Mungu mbele ya Mungu, watu wanaomtamani Mungu. Ni watu walio watulivu tu mbele ya Mungu ndio wanaotilia maanani maisha, wanaotilia maanani ushirika katika roho, walio na kiu ya maneno ya Mungu, na wanaofuatilia ukweli. Wale wote wasiotilia maanani kutulia mbele ya Mungu, wasiofanya mazoezi ya kuwa watulivu mbele ya Mungu ni watu ovyo ambao wamejifunga kabisa kwa dunia, wasio na uzima; hata wakisema wanaamini katika Mungu wanaunga mkono kwa maneno matupu tu. Wale ambao Mungu hukamilisha na kufanya kamili hatimaye ni watu wanaoweza kuwa watulivu mbele ya Mungu. Kwa hivyo, watu walio watulivu mbele ya Mungu ni watu walioneemeshwa na baraka nyingi. Watu ambao mchana hutumia muda mchache kula na kunywa maneno ya Mungu, ambao wameshughulika kabisa na mambo ya nje, na hawatilii maanani kuingia katika uzima wote ni wanafiki wasiokuwa na matarajio ya kuendelea katika siku za usoni. Ni wale wanaoweza kutulia mbele ya Mungu na kushiriki kwa uhalisi na Mungu ndio watu wa Mungu.

Kuja mbele ya Mungu kukubali maneno Yake kama uzima wako, lazima kwanza uwe mtulivu mbele ya Mungu. Ni wakati unapokuwa tu mtulivu mbele ya Mungu ndio Mungu atakupata nuru na kukufanya uelewe. Kadri watu wanavyokuwa watulivu zaidi mbele ya Mungu, ndivyo wanavyoweza kupata nuru na mwangaza wa Mungu zaidi. Haya yanawahitaji watu kuwa na uchaji Mungu na imani. Ni hivyo tu ndivyo wanaweza kutimiza ukamilifu. Zoezi la msingi la kuingia katika maisha ya kiroho ni kuwa mtulivu mbele ya Mungu. Mazoezi yako yote ya kiroho yatafaa tu ikiwa unatuliza mbele ya Mungu. Ikiwa huwezi kuutuliza moyo wako mbele ya Mungu huwezi kupokea kazi ya Roho Mtakatifu. Ikiwa moyo wako umetulia mbele ya Mungu haijalishi unachofanya basi wewe ni mtu unayeishi mbele ya Mungu. Ikiwa moyo wako umetulia mbele ya Mungu na unasonga karibu na Mungu haijalishi unachofanya, hii inathibitisha kuwa wewe ni mtu uliye mtulivu mbele ya Mungu. Unapozungumza na wengine, unapotembea, unaweza kusema, “Moyo wangu unasonga karibu na Mungu, na haulengi mambo ya nje, na naweza kutulia mbele ya Mungu.” Huyu ni mtu aliyetulia mbele ya Mungu. Usiingiliane na vitu vinavyoweza kuelekeza moyo wako kwa mambo ya nje, na usiingiliane na watu wanaoweza kuondoa moyo wako kwa Mungu. Achana na chochote kile kinachoweza kuvuta moyo wako usiwe karibu na Mungu, au kukaa mbali nacho. Njia hiyo ni ya manufaa zaidi kwa maisha yako. Huu ndio wakati wa kazi kuu ya Roho Mtakatifu. Ni wakati ambao Mungu Mwenyewe anawakamilisha watu. Ikiwa kwa wakati huu huwezi kutulia mbele ya Mungu basi wewe si mtu unayerudi mbele ya kiti cha enzi cha Mungu. Ikiwa unafuatilia vitu badala ya Mungu hakuna uwezekano wa kukamilishwa na Mungu. Wale ambao leo wanaweza kusikia matamshi kama haya kutoka kwa Mungu na bado hawawezi kutulia mbele ya Mungu ni watu wasiopenda ukweli, watu wasiompanda Mungu. Ikiwa hutajitoa sasa utafanya hivyo lini? Kujitoa mwenyewe ni kuutuliza moyo wako mbele ya Mungu. Huku ni kujitoa kwa halisi. Yeyote anayetoa moyo wake kwa Mungu sasa kwa kweli bila shaka anaweza kukamilishwa na Mungu. Hakuna chochote, haijalishi ni nini, kinaweza kukusumbua, ikiwa ni cha kukupogoa, au kukushughulikia, au ikiwa wewe hukutana na kuvunjwa moyo au kutofaulu, moyo wako unapaswa kila mara kutulia mbele ya Mungu. Haijalishi watu wanakutendea vipi, moyo wako unapaswa kutulia mbele ya Mungu. Haijalishi unakabiliwa na mazingira gani, iwe ni dhiki, taabu, au mateso, au ikiwa aina nyingi ya majaribio yanakukumba, moyo wako unapaswa kila mara kutulia mbele ya Mungu. Hii ni njia ya kukamilishwa. Ikiwa tu mmetulia kwa kweli mbele ya Mungu ndipo mtaelewa kuhusu maneno ya sasa ya Mungu, kutenda kwa usahihi zaidi mwanga na kupata nuru kwa Roho Mtakatifu na kutopotoka, kuweza kuelewa dhahiri zaidi makusudi ya Mungu na kuwa na mwelekeo wazi zaidi katika huduma yako, kuweza kuelewa kwa usahihi zaidi mguso na uongozi wa Roho Mtakatifu na kuwa na uhakika wa kuishi chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Haya ndiyo matokeo ambayo kuwa mtulivu kwa kweli mbele ya Mungu hutimiza. Wakati watu hawaelewi kuhusu maneno ya Mungu, hawana njia ya kutenda, hawawezi kuyaelewa makusudi

ya Mungu, au hawana kanuni za kutenda, hii ni kwa sababu mioyo yao haijatulia mbele ya Mungu. Kusudi la kuwa mtulivu mbele ya Mungu ni kuwa mwenye ari na wa vitendo na kutafuta usahihi na uangavu katika maneno ya Mungu, hatimaye kutimiza kufahamu ukweli na kumjua Mungu.

Ikiwa moyo wako hauwezi siku zote kutulia mbele ya Mungu, Mungu hawezi kukukamilisha. Ikiwa mtu hana nia iliyo sawa na kukosa moyo, na watu wasio na mioyo hawawezi kutulia mbele ya Mungu. Hawajui ni kazi kiasi gani ambayo Mungu hufanya au kiasi gani Yeye husema, wala hawajui namna ya kuyaweka katika vitendo. Je, hawa si watu wasio na mioyo? Watu wasio na mioyo wanaweza kutulia mbele ya Mungu? Mungu hawezi kuwakamilisha watu wasio na mioyo, nao wako miongoni mwa wanyama. Mungu amenena wazi sana na kikamilifu, ilhali moyo wako bado hauwezi kuisimuliwa na bado huwezi kutulia mbele ya Mungu; je, huku sio kuwa mnyama? Watu wengine hupotoka katika kufanya mazoezi ya kutulia mbele ya Mungu. Ikiwa ni wakati wa kupika hawapiki, na ikiwa ni wakati wa kufanya kazi hawafanyi kazi, lakini wanaendelea tu kuomba na kutafakari. Kutulia mbele ya Mungu hakumaanishi kutopika au kutofanya kazi, wala kuyapuuza maisha, lakini kuweza kuutuliza moyo wa mtu mbele ya Mungu, kuweza kuweka nafasi ya Mungu ndani ya moyo wa mtu katika hali zote za kawaida. Unapomba, piga magoti chini vizuri mbele ya Mungu kuomba; unapofanya kazi au kutayarisha chakula, tuliza moyo wako mbele ya Mungu, tafakari maneno ya Mungu au imba nyimbo za dini. Haijalishi ni mazingira gani uko ndani, una njia ya kufanya mazoezi, fanya kila uwezalo kuwa karibu na Mungu, fanya kila uwezalo kuutuliza moyo wako mbele ya Mungu. Hali zinaporuhusu, omba kwa nia moja; hali zisiporuhusu, mkaribie Mungu ndani ya moyo wako unapofanya kazi hiyo kwa mikono yako. Unapoweza kula na kunywa maneno ya Mungu basi kula na kunywa maneno ya Mungu; unapoweza kuomba basi omba; unapoweza kumtafakari Mungu basi mtafakari Yeye; fanya kila uwezalo kujizoeza kwa ajili ya kuingia kwa kutegemea mazingira yako. Watu wengine wanaweza kutulia mbele ya Mungu wakati hakuna kinachotokea, lakini punde tu jambo hufanyika mioyo yao hulifuatilia. Huko si kutulia mbele ya Mungu. Njia sahihi ya kupata uzoefu ni kwamba moyo wa mtu usimwache Mungu kwa hali yoyote ile, au kuhisi kusumbuliwa na watu, matukio, au mambo ya nje: Huyu ni mtu ambaye ametulia kweli mbele ya Mungu. Watu wengine husema kwamba wanapomba katika mikutano mioyo yao huweza kutulia mbele ya Mungu, lakini wakiwa katika ushirika hawawezi kutulia mbele ya Mungu na mawazo yao hayadhibitiki. Huku si kutulia mbele ya Mungu. Watu wengi sana wakati huu wako katika hali hii, na mioyo yao haiwezi kila mara kutulia mbele ya Mungu. Kwa hiyo mnahitaji kuongeza juhudi zaidi katika kujizoeza katika eneo hili, kuingia hatua kwa hatua katika njia sahihi ya uzoefu wa maisha na kutembea juu ya njia ya kukamilishwa na Mungu.

Kuwa Mzingatifu wa Mapenzi ya Mungu ili Upate Utimilifu

Kadiri unavyozingatia mapenzi ya Mungu, ndivyo unavyokuwa na mzigo zaidi; kadiri unavyokuwa na mzigo, ndivyo uzoefu wako utakuwa mwingi zaidi. Unapokuwa mzingatifu wa mapenzi ya Mungu, Mungu atakupa mzigo huu, na Mungu atakupa nuru ya mambo ambayo amekuaminia. Baada ya Mungu kukupa mzigo huu, utaangalia ukweli wa kipengele hiki unapokula na kunywa maneno ya Mungu. Kama una mzigo unaohusiana na hali ya maisha ya ndugu, huu ni mzigo ulioaminiwa kwako na Mungu, na sala zako za kila siku daima zitaubeba mzigo huu. Kile ambacho Mungu hufanya kimeaminiwa kwako, uko radhi kutekeleza kile ambacho Mungu anataka kufanya, na hivi ndivyo inavyomaanisha kuuchukua mzigo wa Mungu kama wako. Wakati huu, kula na kunywa kwako maneno ya Mungu kutalenga masuala katika vipengele hivi, na utafikiri: Nitayatatuaje masuala haya? Nitawaruhusu vipi ndugu kufunguliwa, wawe na furaha katika nafsi zao? Utalenga kusuluhisha masuala haya unapokuwa katika ushirika, utalenga kula na kunywa maneno yanayohusiana na masuala haya wakati ambapo unakula na kunywa maneno ya Mungu, utakuwa ukila na kunywa maneno ya Mungu na wakati huo ukiubeba mzigo huu, na utaelewa matakwa ya Mungu. Wakati huu, utakuwa wazi zaidi kuhusu njia ya kutembelea. Huku ni kupata nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu kunakosababishwa na mzigo wako, na huku ni Mungu kukupa mwongozo Wake. Kwa nini Nasema hili? Ikiwa huna mzigo, basi huzingatii unapokula na kunywa maneno ya Mungu; unapokuwa ukila na kunywa maneno ya Mungu na wakati huo kuubeba mzigo, unakuwa na uwezo wa kuelewa kiini cha maneno ya Mungu, kutafuta njia yako, na kuzingatia mapenzi ya Mungu. Kwa hivyo, unapaswa kumsihi Mungu akuongezee mizigo zaidi katika sala zako ili aweze kukuaminia mambo makuu zaidi, unaweza vyema zaidi kupata njia ya utendaji mbele, unakuwa wa kufaa zaidi katika kula na kunywa maneno ya Mungu, unakuwa na uwezo wa kuelewa kiini cha maneno Yake, na unaweza zaidi kukubali kuguswa hisi na Roho Mtakatifu.

Kula na kunywa maneno ya Mungu, kufanya maombi, kukubali mzigo wa Mungu, kukubali Anachokuaminia—haya yote ni kwa ajili ya kuwa na njia mbele yako. Kadiri unavyozidi kuwa na mzigo mwingi wa agizo la Mungu, ndivyo itakavyokuwa rahisi zaidi kwako kufanywa mtimilifu na Mungu. Wengine hawako tayari kushirikiana katika kumtumikia Mungu hata wakati ambapo wameshurutishwa; hao ni watu wavivu ambao hutamani kufurahia faraja. Kadiri unavyotakiwa kushirikiana katika kumhudumia Mungu, ndivyo utakavyopata uzoefu zaidi. Kwa sababu una mizigo zaidi na una uzoefu zaidi, utakuwa na nafasi zaidi ya kufanywa mtimilifu. Kwa hivyo, ikiwa unaweza kumhudumia Mungu kwa uaminifu utazingatia mzigo wa Mungu, na kwa njia hii utakuwa na nafasi nyingi zaidi za kufanywa mtimilifu na Mungu. Kundi kama hili la watu linafanywa kamilifu na Mungu wakati huu. Kadiri Roho Mtakatifu anavyokugusa hisia, ndivyo utakavyotenga muda zaidi wa kuzingatia mzigo wa Mungu, ndivyo utakavyofanywa

mtimilifu na Mungu zaidi, ndivyo Mungu atakavyokupata zaidi, na mwishowe, utakuwa mtu anayetumiwa na Mungu. Sasa, kuna baadhi ambao hawalibebi kanisa mzigo. Watu hawa ni wazembe na wenye ubwege, na wanajali tu miili yao. Wao ni wenye ubinafsi sana na ni vipofu pia. Hutakuwa na mzigo wowote ikiwa huna uwezo wa kuona suala hili kwa dhahiri. Kadiri unavyozidi kuwa mzingatifu wa mapenzi ya Mungu, ndivyo mzigo ambao Mungu atakuaminia utakavyozidi kuwa mzito. Watu wenye ubinafsi hawako tayari kuyapitia mambo kama haya, na hawako radhi kulipa gharama, na kwa sababu hiyo watakosa nafasi ya kufanywa wakamilifu na Mungu. Je, si huku ni kujiumiza? Ikiwa wewe ni mtu ambaye ni mzingatifu wa mapenzi ya Mungu, utakuza mzigo wa kweli kwa ajili ya kanisa. Kwa kweli, badala ya kuuita huu mzigo wa kanisa, badala yake ni mzigo wa maisha yako, kwa sababu mzigo unaokuza kwa ajili ya kanisa ni kwa ajili yako kufanywa mtimilifu na Mungu kwa kupitia uzoefu kama huu. Kwa hivyo, yeyote anayelibeba kanisa mzigo mzito zaidi na yeyote abebaye mzigo wa kuingia katika maisha watakuwa wale ambao wanafanywa watimilifu na Mungu. Je, umeona hili kwa dhahiri? Ikiwa kanisa unaloshiriki limetawanyika kama mchanga, lakini bado huna wahaka wala wasiwasi, na hata unajitia hamnazo wakati kina ndugu zako hawali au kunywa maneno ya Mungu kwa kawaida, basi huibebi mizigo yoyote. Watu kama hawa hawapendwi na Mungu. Wale wanaopendwa na Mungu huwa na shauku na kiu ya haki na ni wazingatifu wa mapenzi Yake. Kwa hivyo mnapaswa kuwa wazingatifu wa mzigo wa Mungu sasa. Hupaswi kusubiri tabia ya Mungu yenye haki ifunuliwe kwa watu wote kabla ya wewe kuwa mzingatifu wa mzigo wa Mungu. Je, si muda utakuwa umeshapita wakati huo? Sasa ni nafasi nzuri ya kufanywa mtimilifu na Mungu. Ukiruhusu nafasi hii ipotee, utajuta katika maisha yako yote, kama vile Musa alivyoshindwa kuingia katika nchi nzuri ya Kanani na alijuta katika maisha yake yote, akifa kwa majuto. Mara tu Mungu ameifichua tabia Yake yenye hakikwa watu wote, utajawa na majuto. Hata kama Mungu hakuadibu, utajiadibu kutokana na majuto yako mwenyewe. Wengine hawaridhishwi na hili. Ikiwa huamini, basi subiri uone. Watu wengine watatumika kama utimizaji wa maneno haya. Je, uko tayari kuwa sadaka ya dhabihu kwa maneno haya?

Usipotafuta fursa za kufanywa mtimilifu na Mungu, na usipojitahidi kuwa mbele katika kutafuta kwako kukamilishwa, basi hatimaye utajawa na majuto. Sasa ni fursa nzuri ya kufanywa mtimilifu—huu ni wakati mzuri. Usipotafuta kwa bidii kufanywa mtimilifu na Mungu, mara tu kazi Yake itakapokuwa imekamilika utakuwa umechelewa—utakuwa umekosa fursa hii. Bila kujali jinsi matarajio yako yalivyo makuu, ikiwa Mungu hatendi kazi tena, bila kujali jitihada unazotia, hutaweza kamwe kufanywa mtimilifu. Lazima uchukue fursa hii na ushirikiane kupitia huku Roho Mtakatifu akiwa anafanya kazi Yake kuu. Ukipoteza fursa hii, hutapewa nyingine bila kujali juhudi unazotia. Watu wengine hulika: “Mungu, niko radhi kuzingatia mzigo Wako, na niko radhi kuyaridhisha mapenzi Yako.” Ilhali hawana njia ya utendaji, kwa hivyo mizigo yao

haitadumu. Ikiwa kuna njia, utapata uzoefu hatua kwa hatua, na itakuwa na muundo na ratiba. Baada ya mzigo mmoja kukamilika, mwingine unakabidhiwa kwako. Kupitia kuongezeka kwa uzoefu wako wa maisha, mizigo yako inakua pia. Watu wengine hubeba mzigo tu wanapoguswa hisia na Roho Mtakatifu, na baada ya kipindi cha muda, hawaubebi tena mizigo yoyote wakati ambapo hakuna njia ya utendaji. Huwezi kupata mizigo kwa kula na kunywa tu maneno ya Mungu. Kwa kuelewa ukweli mwingi, utapata umaizi, utakuwa na uwezo wa kutatua matatizo kwa kutumia ukweli, na ufahamu mzuri zaidi wa maneno ya Mungu na mapenzi ya Mungu. Kwa mambo haya, utakuza mizigo, na utaweza kufanya kazi nzuri mara tu unapokuwa na mzigo. Ikiwa una mzigo tu lakini huna ufahamu wa ukweli ulio wazi, hiyo pia haitasaidia. Lazima wewe mwenyewe uwe na uzoefu wa maneno ya Mungu, na ujue jinsi ya kuyatenda, na lazima kwanza uingie katika hali halisi kabla ya kuwakimu wengine, kuwaongoza wengine, na kufanywa mtimilifu na Mungu.

Katika “Njia ... (4)”, imeandikwa kwamba ninyi nyote ni watu wa ufalme, waliojaaliwa na Mungu kabla ya enzi, na haliwezi kuchukuliwa na mtu yeyote. Pia inasema kwamba Mungu anataka kila mtu atumiwe na Mungu na kufanywa mtimilifu na Mungu, na Anawataka kusimama kama watu Wake, na kwamba kuwa tu watu wa Mungu kutaweza kutimiza mapenzi Yake. Mlikuwa na ushirika juu ya suala hili wakati huo, ushirika juu ya njia ya kuingia kulingana na vigezo kwa watu wa Mungu, kwa hivyo kazi iliyofanywa na Roho Mtakatifu wakati huo ilikuwa kumwondoa kila mtu kutoka kwa hali yake mbaya na kumwongoza katika hali nzuri. Wakati huo, mwenendo wa kazi ya Roho Mtakatifu ulikuwa kumfanya kila mtu afurahie maneno ya Mungu kama watu wa Mungu, na kuruhusu kila mmoja wenu kuelewa kwa wazi kwamba ninyi ni watu wa Mungu waliojaaliwa kabla ya enzi, na Shetani hawezi kukuchukua. Kwa hivyo, nyote mliomba, “Mungu! Niko tayari kuwa mmoja wa watu Wako, kwa sababu tumejaaliwa na Wewe kabla ya enzi, kwa sababu umetupa haya. Tuko tayari kuchukua nafasi hii na kukuridhisha.” Ulipomwomba kwa namna hiyo, Roho Mtakatifu angekusisimua—huo ndio mwelekeo wa kazi ya Roho Mtakatifu. Katika kipindi hiki cha muda ni kuomba na kufanya mazoezi ya kutuliza moyo wako mbele ya Mungu ili uweze kufuatilia maisha na kufuatilia kuingia katika mafunzo ya ufalme. Hii ndiyo hatua ya kwanza. Kwa sasa, kazi ya Mungu ni kuwa kila mtu aingie kwenye njia sahihi, awe na maisha ya kawaida ya kiroho na uzoefu wa kweli, aongozwe na Roho Mtakatifu, na kwa msingi wa msingi huu, kukubali kile kilichowekwa na Mungu. Kusudi la kuingilia katika mafunzo ya ufalme ni kuruhusu kila neno lenu, kila tendo, kila mwendo na kila mawazo na wazo la kuingilia katika maneno ya Mungu, kuwawezesha kuguswa na Mungu mara nyingi zaidi na kukuza upendo kwa Mungu na kukuza mzigo mzito zaidi kwa ajili ya mapenzi ya Mungu, ili kila mtu awe kwenye njia ya kufanywa mtimilifu na Mungu, na kila mtu awe kwenye njia sahihi. Mara unapokuwa kwenye njia ya kufanywa mtimilifu na Mungu, basi uko kwenye

njia sahihi. Wakati ambapo mawazo yako na dhana zako pamoja na malengo yako mabaya yanaweza kurekebisha na unaweza kugeuka kutoka katika kuzingatia mwili wako hadi kuzingatia mapenzi ya Mungu, na wakati ambapo malengo mabaya yanajitokeza na unaweza kutosumbuliwa nayo na kutenda kwa mujibu wa mapenzi ya Mungu—ikiwa unaweza kufikia mageuzo hayo, basi uko kwenye njia sahihi ya uzoefu wa maisha. Utendaji wako wa sala unapokuwa kwenye njia sahihi, hapo ndipo utakapoongozwa na Roho Mtakatifu katika sala zako. Kila wakati unapoomba, utaguswa hisia na Roho Mtakatifu; kila wakati utakapoomba, utakuwa na uwezo wa kutuliza moyo wako mbele ya Mungu. Kila wakati ambapo unakula na kunywa kifungu cha neno la Mungu, ikiwa unaweza kuelewa kazi ambayo anafanya sasa, na unaweza kujua jinsi ya kuomba, jinsi ya kushirikiana, na jinsi ya kuingia ndani, huku tu ndiko kufikia matokeo kutokana na kula na kunywa maneno ya Mungu. Unapoweza kupata njia ya kuingia kutoka kwa maneno ya Mungu, na unaweza kuelewa mienendo ya sasa ya kazi ya Mungu na mwenendo wa kazi ya Roho Mtakatifu kwa maneno Yake, hii inaonyesha kwamba wewe u kwenye njia sahihi. Ikiwa hujafahamu hoja muhimu unapokula na kunywa maneno ya Mungu, ikiwa huwezi kupata njia ya kutenda baada ya kula na kunywa maneno ya Mungu, inaonyesha kuwa bado hujui jinsi ya kula na kunywa maneno Yake na kwamba wewe hujapata njia au kanuni ya kula na kunywa maneno Yake. Ikiwa hamjalewa kazi iliyofanywa na Mungu kwa sasa, hutaweza kukubali Agizo la Mungu. Kazi ambayo sasa inafanywa na Mungu ni ile wanapaswa kuingia ndani na kuwa na ujuzi kuhusu kwa sasa. Je, mnaelewa mambo haya?

Ukila na kunywa maneno ya Mungu kwa njia inayofaa, maisha yako ya kiroho yanakuwa ya kawaida, na bila kujali ni majaribu gani unayoweza kukabili, ni hali gani unazoweza kukumbana nazo, ni magonjwa gani ya kimwili unayoweza kuvumilia, ni mafarakano gani kutoka kwa ndugu au ni shida zipi za kifamilia unazoweza kupitia, unaweza kula na kunywa maneno ya Mungu kwa kawaida, kuomba kawaida, na kuendelea na maisha yako ya kanisa kawaida; ikiwa unaweza kutimiza haya yote, itaonyesha kuwa uko kwenye njia sahihi. Watu wengine ni dhaifu sana na hawana uvumilivu. Wanapokutana na kizuizi kidogo, wao hunung'unika na kuwa hasi. Ufuatiliaji wa ukweli unahitaji uvumilivu na uamuzi. Ikiwa huwezi kuyakidhi mapenzi ya Mungu wakati huu, lazima uweze kujidharau, kwa kimya kuwa na uamuzi ndani ya moyo wako kwamba utayaridhisha mapenzi ya Mungu wakati mwingine ujao. Ikiwa wakati huu hukuwa mzingatifu wa mzigo wa Mungu, unapaswa kuwa na azimio la kuasi dhidi ya mwili wakati ambapo unakabiliwa na kile kikwazo sawa katika siku zijazo, na kukusudia kuyaridhisha mapenzi ya Mungu. Hivi ndivyo unavyokuwa wa kustahili sifa. Watu wengine hata hawajui kama mawazo yao na dhana zao ni sawa—watu kama hao ni wapumbavu! Ikiwa ungependa kuuhini moyo wako na kuasi dhidi ya mwili, lazima kwanza ujue kama malengo yako ni sahihi, na hapo tu ndipo utaweza kuuhini moyo wako. Ikiwa hujui ikiwa nia yako ni sawa,

unaweza kuuhini moyo wako na kuasi dhidi ya mwili? Hata ukiasi, unafanya hivyo kwa njia ya kuchanganyikiwa. Unapaswa kujua jinsi ya kuasi dhidi ya malengo yako potovu; hii ndiyo maana ya kuasi dhidi ya mwili. Unapojua kwamba malengo yako, mawazo yako na dhana zako si sahihi, unapaswa kukimbilia kurudi nyuma na kutembea kwenye njia sahihi. Tatua tatizo hili kwanza na ujifunze kufikia uingiaji kwa namna hii, kwa sababu unajua bora zaidi kama nia yako ni sawa au la. Wakati malengo mabaya yanarekebisha na ni kwa ajili ya Mungu, basi umefikia lengo la kuuhini moyo wako.

Cha muhimu kwenu sasa ni kuwa na maarifa ya Mungu, kuwa na maarifa ya kazi ya Mungu, na lazima ujue jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi Yake kwa mwanadamu; huu ndio ufunguo wa kuingia kwenye njia sahihi. Itakuwa rahisi kwako kuingia kwenye njia sahihi baada ya kufahamu ufunguo huu. Unamwamini Mungu na kumjua Mungu, ambayo inaonyesha kwamba imani yako kwake ni ya kweli. Ikiwa utaendelea kupata uzoefu mpaka mwisho lakini bado huna uwezo wa kumjua Mungu, basi wewe hakika ni mtu anayempinga Mungu. Wale ambao huamini tu katika Yesu Kristo lakini hawaamini katika Mungu mwenye mwili wa leo wote wamehukumiwa. Wote ni Mafarisayo wa wakati wa sasa, kwa kuwa hawamtambui Mungu wa leo; wote wanampinga Mungu. Bila kujali imani yao katika Yesu ni ya kujitolea kiasi gani, itakuwa bure; hawatapata sifa ya Mungu. Wote wanaosema kuwa wanaamini katika Mungu ilhali hawana maarifa ya kweli ya Mungu katika mioyo yao ni wanafiki!

Ili kutafuta kufanywa mtimilifu na Mungu, mtu lazima kwanza aelewe maana ya kufanywa mtimilifu na Yeye, ni hali gani ambazo mtu anapaswa kumiliki ili kufanywa mtimilifu, na kisha kutafuta njia ya kutenda mara mtu ameelewa mambo kama hayo. Mtu lazima awe na ubora fulani wa tabia ili afanywe mtimilifu na Mungu. Wengi wenu hawana ubora muhimu wa tabia, ambao unahitaji wewe kulipa gharama fulani na jitihada zako za nafsi. Kadiri ubora wako wa tabia unavyozidi kuwa wa chini, ndivyo lazima utie juhudi zaidi za binafsi. Kadiri ufahamu wako wa maneno ya Mungu ulivyo mkuu na kadiri unavyoyatia kwenye matendo, ndivyo unavyoweza kuingia kwenye njia ya kufanywa mtimilifu na Mungu haraka. Kupitia katika maombi, unaweza pia kufanywa mtimilifu katika maombi; pia unaweza kufanywa mtimilifu kwa kula na kunywa maneno ya Mungu, kuelewa kiini cha maneno hayo, na kuishi kwa kudhihirisha ukweli wa maneno ya Mungu, unaweza kufanywa kuwa mtimilifu. Kupitia uzoefu wa maneno ya Mungu kila siku, unapaswa kujua kile unachokosa ndani yako, na, zaidi ya hayo, unapaswa kujua dosari yako kubwa na upungufu wako, na umwombe na kumsihi Mungu. Kwa kufanya hivyo, utafanywa mtimilifu polepole. Njia za kufanywa mtimilifu: kuomba, kula na kunywa maneno ya Mungu, kuelewa kiini cha maneno ya Mungu, kuingia katika uzoefu wa maneno ya Mungu, kuja kujua kinachokosa ndani yako, kuitii kazi ya Mungu, kuzingatia mzigo wa Mungu na kuunyima mwili kwa kupitia upendo wako kwa Mungu, na kuwa na ushirika wa mara kwa mara na ndugu,

ambayo yanaboresha uzoefu wako. Iwe ni maisha ya jumuiya au maisha yako binafsi, na iwe ni makusanyiko makubwa au madogo, yote yanaweza kukuwezesha kupata uzoefu na kupata mafunzo ili moyo wako uwe na utulivu mbele ya Mungu na kurudi kwa Mungu. Haya yote ni mchakato wa kufanywa mtimilifu. Kuyapitia maneno ya Mungu ambayo yamesemwa kunamaanisha kuwa na uwezo wa kwa kweli kuyaonja maneno ya Mungu na kuyaruhusu yaweze kuishi kwa kudhihirishwa ndani yako ili uwe na imani kubwa na upendo kwa Mungu. Kupitia njia hii, utaondoa tabia potovu ya kishetani polepole, utaachana na motisha isiyofaa polepole, na kuishi kwa kudhihirisha mfano wa mtu wa kawaida. Kadiri upendo kwa Mungu ndani yako unavyozidi kuwa mkuu—yaani, kadiri unavyozidi kufanywa mtimilifu na Mungu mara nyingi—ndivyo unayopotoshwa na Shetani kwa kiasi kidogo. Kupitia uzoefu wako wa vitendo, utaingia kwenye njia ya kufanywa mtimilifu polepole. Hivyo, ikiwa unataka kufanywa mtimilifu, kuzingatia mapenzi ya Mungu na kuyapitia maneno ya Mungu hasa ni muhimu sana.

Mungu Anawakamilisha Wale Wanaoupendeza Moyo Wake

Kundi la watu ambao Mungu anataka kupata sasa ni wale ambao wanajitahidi kushirikiana na Mungu, wanaoweza kuiheshimu kazi Yake, na wanaoamini kuwa maneno Anayonena Mungu ni ya kweli, wale wanaoweza kuweka mahitaji ya Mungu katika vitendo. Ni wale walio na uelewa wa kweli katika mioyo yao. Ni hao ndio wanaoweza kukamilishwa, na wale ambao bila shaka watatembea katika njia ya ukamilisho. Wale wasio na uelewa wa wazi wa kazi ya Mungu, wale wasiokula na kunywa neno la Mungu, wale wasiotilia maanani neno la Mungu, na wale wasio na upendo wowote kwa Mungu katika mioyo yao. Wale walio na shaka na Mungu mwenye mwili, wasio na uhakika juu Yake, wasiyoachukulia maneno ya Mungu kwa uzito na ambao daima humdanganya Mungu ni watu wanaompinga Mungu na ni wa Shetani; hakuna njia ya kukamilisha watu kama hao.

Kama unataka kufanywa mkamilifu, lazima kwanza uwe na neema ya Mungu, kwa sababu Mungu anawakamilisha wale ambao Amewapa neema, wale wanaoupendeza moyo Wake. Kama unataka kuupendeza moyo wa Mungu, lazima uwe na moyo unaotii kazi Yake yote, lazima ujitahidi kuufuata ukweli, na lazima ukubali uchunguzi wa Mungu katika kila kitu. Je, kila kitu unachofanya kimepitia uchunguzi wa Mungu? Je, nia yako iko sawa? Kama nia yako iko sawa, Mungu Atakubaliana nawe; kama nia yako sio sawa, hii inathibitisha kwamba kile moyo wako unapenda sio Mungu, ni mwili na Shetani. Kwa hiyo, lazima utumie maombi kama njia ya kukubali uchunguzi wa Mungu katika kila. Unapoomba, ingawa Mimi mwenyewe sisimami mbele yako, Roho Mtakatifu yuko pamoja nawe, na unaomba kwa Mimi mwenyewe na Roho wa Mungu. Kwa nini unaamini katika mwili huu? Unaamini kwa sababu Yuko na Roho wa Mungu. Je, ungemwamini mtu huyu ikiwa hangekuwa na Roho wa Mungu. Unapoamini katika mtu huyu,

unaamini katika Roho wa Mungu. Unapomwogopa mtu huyu, unamwogopa Roho wa Mungu. Imani katika Roho wa Mungu ni imani katika mtu huyu, imani katika mtu huyu pia ni imani katika Roho wa Mungu. Unapoomba, unahisi Roho wa Mungu akiwa pamoja nawe, Mungu yuko mbele yako, kwa hivyo unamwomba Roho wa Mungu. Leo, watu wengi wanaogopa sana kuyaleta matendo yao mbele za Mungu, na ingawa unaweza kuudanganya mwili wa Mungu, huwezi kumdanganya Roho wa Mungu. Yale yote ambayo hayawezi kustahimili uchunguzi wa Mungu hayakubaliani na ukweli nayo lazima yawekwe kando, ama unatenda dhambi dhidi ya Mungu. Kwa hivyo, haijalishi kama ni wakati unaomba, unaponena na kushiriki na ndugu na dada zako, ama unapofanya wajibu wako na kufanya biashara yako, lazima uweke moyo wako mbele za Mungu. Unapoitimiza kazi yako, Mungu yuko nawe, na bora nia yako iwe sawa, nayo iwe kwa ajili ya kazi ya nyumba ya Mungu, Atakubali kila kitu ufanyacho, kwa hivyo ni lazima uweke bidii kwa dhati kujishughulisha na kuitimiza kazi yako. Unapoomba, kama una upendo kwa Mungu katika moyo wako, na kama unatafuta utunzaji wa Mungu, ulinzi, na uchunguzi, kama haya ndio nia yako, maombi yako yatafaulu. Unapoomba katika mikutano, ndivyo unafaa kufungua moyo wako na kuomba Mungu, ambia Mungu kile kilicho moyoni mwako, na bila kuongea uongo, basi maombi yako yatafaulu. Kama unampenda Mungu moyoni mwako kwa dhati, basi fanya kiapo kwa Mungu: “Mungu, uliye mbinguni na nchini na vitu vyote, naapa Kwako: Hebu Roho Wako achunguze kila kitu ninachofanya na unilinde na kunijali kila wakati. Kinafanya kila kitu nifanyacho kiweze kusimama katika uwepo Wako. Ikiwa moyo wangu utawahi kukoma kukupenda ama kukusaliti Wewe, nipe adhabu Yako na laana kali zaidi. Usinisamehe katika dunia hii ama inayofuata!” Unaweza kuthubutu kula kiapo kama hiki? Kama huwezi, hii inadhibitisha kuwa wewe ni mwoga, na kwamba bado unajipenda. Je, mnao uamuzi huu? Kama kweli huu ndio uamuzi wako, lazima ufanye kiapo hiki. Kama una azimio la kula kiapo kama hiki, Mungu ataridhisha uamuzi wako. Unapoapa kwa Mungu, Mungu anasikiza. Mungu Anaamua kama wewe ni mwenye dhambi ama mwenye haki kupitia maombi yako na matendo yako. Huu sasa ndio mchakato wa kukukamilisha, na kama kweli unayo imani katika kukamilishwa kwako na Mungu, basi utaleta kila kitu ufanyacho mbele za Mungu na kuukubali uchunguzi Wake; ukifanya kitu kinachoasi sana ama ukimsaliti Mungu, basi atatimiza kiapo chako, na kisha haijalishi kitakachokufanyikia, iwe kuangamia ama kuadibu, ni shida yako mwenyewe. Ulikula kiapo, basi lazima ukitekeleze. Ukila kiapo, lakini ukose kukitekeleza, utaangamia. Kwa kuwa unakula kiapo, Mungu atatimiza kiapo chako. Wengine wanaogopa baada ya kuomba, na kusema, “Ee, jamani, nafasi yangu katika ufisadi imepotea, nafasi yangu kufanya mambo maovu imepotea, nafasi yangu ya kujiingiza katika ulafi wangu wa kidunia imepotea!” Watu hawa bado wanaipenda dunia na dhambi, nao ni hakika wataangamia.

Kuwa muumini katika Mungu kunamaanisha kuwa kila kitu ufanyacho lazima kiletwe

mbele za Mungu na kupitia uchunguzi wa Mungu. Kama kile ufanyacho kinaweza kuletwa mbele za Roho wa Mungu lakini sio mbele ya mwili wa Mungu, hii inadhibitisha kuwa hujajitiisha katika uchunguzi wa Roho wa Mungu. Roho wa Mungu ni nani? Mtu huyu aliyeshuhudiwa na Mungu ni nani? Je, Wote si sawa? Wengi Huwaona kama nafsi mbili tofauti, wakiamini kwamba Roho wa Mungu ni Roho wa Mungu, naye mtu anayeshuhudiwa na Mungu ni binadamu tu. Lakini, je, hujakosea? Je, mtu huyu anafanya kazi kwa niaba ya nani? Wale ambao hawaujui mwili wa Mungu hawana uelewa ya kiroho. Roho wa Mungu na mwili Wake ni mmoja, kwa sababu Roho wa Mungu anatokea kwa mwili. Kama mtu huyu si mwema kwako, Roho wa Mungu Atakuwa mwema? Ni nini kimekuchanganya? Leo, hakuna asiyekubali uchunguzi wa Mungu anaweza kupokea idhini ya Mungu, na yeyote asiyemjua Mungu mwenye mwili hawezi kukamilishwa. Jiangalie nawe ujiulize kama kila kitu unachofanya kinaweza kuletwa mbele ya Mungu. Iwapo huwezi kuleta kila kitu unachofanya mbele za Mungu, hii inaonyesha kuwa wewe ni mtenda maovu. Je, watenda maovu wanaweza kufanywa wakamilifu? Kila kitu unachofanya, kila tendo, kila nia, na kila jibu lazima kiletwe mbele za Mungu. Hata maisha yako ya kawaida ya kiroho—maombi yako, ukaribu wako kwa Mungu, jinsi unavyokula na kunywa maneno ya Mungu, ushirika wako na kina ndugu zako na maisha yako ndani ya kanisa—na huduma yako katika ushirikiano wako vinaweza kuletwa mbele za Mungu ili Yeye avichunguze. Ni matendo kama hayo ndiyo yatakayokusaidia kustawi katika maisha. Mchakato wa kukubali uchunguzi wa Mungu ni mchakato wa kutakaswa. Kadri unavyokubali uchunguzi wa Mungu, ndivyo unavyotakaswa zaidi na kadri unavyokubaliana na matakwa ya Mungu, ili kwamba hutajipata katika uasherati, na moyo wako utaishi katika uwepo wa Mungu; kadri unavyokubali uchunguzi wa Mungu, ndivyo unavyomuaibisha Shetani na kuutelekeza mwili. Kwa hivyo, kukubali uchunguzi wa Mungu ni njia ambayo watu wanafaa kutenda. Haijalishi kile unachokifanya, hata katika ushirika na ndugu na dada zako, ukiyaleta matendo yako mbele za Mungu na kutafuta uchunguzi wa Mungu, na kama nia yako ni kumtii Mungu Mwenyewe, unachotenda ni sahihi zaidi. Kama tu wewe ni mtu anayeleta kila kitu anachofanya mbele za Mungu na kukubali uchunguzi wa Mungu ndipo utakapokuwa mtu anayeishi kwa hakika katika uwepo wa Mungu.

Wale wasio na uelewa wa Mungu hawawezi kumtii Mungu kikamilifu. Watu kama hao ni wana wa uasi. Ni wenye kutaka makuu sana, na kuna uasi mwingi sana ndani mwao, kwa hivyo wanajitenga na Mungu na hawana nia ya kukubali uchunguzi wa Mungu. Watu kama hao hawawezi kufanywa wakamilifu na Mungu kwa urahisi. Watu wengine wana uchaguzi katika vile wanavyokula na kunywa neno la Mungu na katika hali yao ya kulikubali. Wanakubali sehemu za neno la Mungu zinazolingana na dhana zao wakikataa zile zisizokubaliana nazo. Je, hawamwasi na kumkataa Mungu kwa uwazi? Kama mtu anaamini katika Mungu kwa miaka

mingi bila kupata uelewa hata kidogo wa Mungu, yeye ni mtu asiyeamini. Wale walio tayari kukubali uchunguzi wa Mungu ni wale wanao tafuta uelewano wa Mungu, walio tayari kukubali neno la Mungu. Ni wale ambao watapokea uridhi wa Mungu na mibaraka, nao ni wale waliobarikiwa zaidi. Mungu analaani wale wasio na nafasi Yake katika mioyo yao. Anawaadibu na kuwaacha watu kama hao. Kama humpendi Mungu, Mungu atakuacha, na kama hutasikia Ninachosema, Naahidi kwamba Roho wa Mungu atakuacha. Jaribu hili iwapo hauniamini! Leo Nawaambia njia ya kufuata, lakini kama utafanya hivyo ni juu yako. Kama huamini hilo, kama hilitii katika vitendo, utaona kama Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani yako au la! Kama hautatafuta uelewano wa Mungu, Roho Mtakatifu hatafanya kazi ndani mwako. Mungu anafanya kazi ndani ya wale wanaotafuta na kulithamini neno la Mungu. Kadri unavyolithamini neno la Mungu, ndivyo Roho wa Mungu atakavyofanya kazi zaidi ndani mwako. Kadri mtu anavyolithamini neno la Mungu, ndivyo nafasi yake ya kukamilishwa na Mungu inavyokuwa kubwa. Mungu anawakamilisha wale ambao wanampenda Yeye kwa kweli. Anawakamilisha wale ambao mioyo yao iko katika amani mbele Yake. Ukiithamini kazi yote ya Mungu, yaani, ukiuthamini mwanga wa Mungu, ukiuthamini uwepo wa Mungu, ukithamini kujali na kuwekwa kwa Mungu, ukithamini jinsi neno la Mungu linakuwa ukweli wako na utoaji wa maisha, unafuata zaidi moyo wa Mungu. Ukiithamini kazi ya Mungu, ukiithamini kazi yote ambayo Mungu Amefanya juu yako, Mungu Atakubariki na kufanya kila kitu kilicho chako kuongezeka. Usipoithamini kazi ya Mungu, Mungu Hatafanya kazi kwako, Atakuruhusu tu nyakati za neema kwa imani yako, ama kukubariki na utajiri kidogo ama usalama kwa familia yako. Lazima utie bidii kuyafanya maneno ya Mungu kuwa ukweli wako ili umridhishe Yeye na kuupendeza moyo Wake, sio tu kutia bidii kufurahia neema ya Mungu. Hakuna kitu muhimu zaidi kwa waumini kama kupokea kazi ya Mungu, kupata ukamilifu, na kuwa wanaofanya mapenzi ya Mungu. Hili ndilo lengo unalofaa kufuata.

Kila ambacho mwanadamu alitafuta katika Enzi ya Neema sasa hakiko tena, kwa sababu kiwango cha juu cha ufuatiliaji; kinachofuatiliwa ni cha juu zaidi na cha vitendo zaidi, linalofuatiliwa linaweza kukidhi zaidi kile ambacho mwanadamu anahitaji ndani. Katika enzi zilizopita, Mungu hakuwafanyia watu kazi kama Afanyavyo leo; Hakunena nao sana jinsi Amenena leo, wala mahitaji Yake kwao hayakuwa ya juu kama ya leo. Kwamba Mungu anainua vitu hivi kwenu kunathibitisha kuwa nia ya mwisho ya Mungu, kumelengwa kwenu, kundi hili. Iwapo kweli unataka kufanywa mkamilifu na Mungu, basi lifuate kama lengo lako kuu. Haijalishi kama unakwenda huku na kule, unajitumia, unatenda wajibu, ama kama umepokea agizo la Mungu, nia daima ni kukamilishwa na kuridhisha mapenzi ya Mungu, kutimiza malengo haya. Mtu akisema kuwa hafuati kukamilishwa na Mungu ama kuingia katika maisha, lakini anafuata tu amani na furaha ya kimwili, basi yeye ni kipofu kabisa. Wale wasiofuata ukweli wa

maisha, lakini wanafuata maisha ya milele pekee katika maisha ya baadaye na usalama katika maisha haya ni vipofu kabisa. Kwa hivyo, kila kitu ufanyacho lazima kifanywe kwa madhumuni ya kufanywa mkamilifu na kupatwa na Mungu.

Kazi ambayo Mungu anafanya kwa watu ni kuwakimu kulingana na mahitaji yao tofauti. Kadri maisha ya mwanadamu yalivyo makubwa, ndivyo anavyohitaji mengi zaidi, na ndivyo anavyotafuta zaidi. Kama katika awamu hii huna harakati, inathibitisha kuwa Roho Mtakatifu amekuacha. Wale wote wanaofuata maisha hawatawahi kuachwa na Roho Mtakatifu, wao hufuata kila wakati, wanatamani kila wakati. Watu kama hao hawatosheki kamwe kupumzika mahali walipo. Kila awamu ya kazi ya Roho Mtakatifu inalenga kufikia athari ndani mwako, lakini ukikua wa kutojali, kama hauhitaji tena, kama huikubali kazi ya Roho Mtakatifu, Yeye atakuacha. Watu wanahitaji uchunguzi wa Mungu kila siku, wanahitaji kupewa kwa wingi kutoka kwa Mungu kila siku. Je, watu wanaweza kuishi bila kula na kunywa neno la Mungu kila siku? Kama mtu anahisi kuwa hawezi kula ama kunywa neno la Mungu vya kutosha, kama analitafuta kila siku na kuwa na njaa na kiu kwake, Roho Mtakatifu atafanya kazi juu yao. Kadri mtu anavyotamani, ndivyo atakavyokuwa na ushirika kuhusu vitu vya hakika. Kadri mtu anavyotafuta ukweli sana, ndivyo maisha yake yanavyokua kwa haraka, yakimpa uzoefu wa hali ya juu na kumfanya tajiri katika nyumba ya Mungu.

Wale Wanaomtii Mungu kwa Moyo wa Kweli Hakika Watapatwa na Mungu

Kazi ya Roho Mtakatifu inabadilika kutoka siku hadi siku, ikipanda juu kwa kila hatua; ufunuo wa kesho unakuwa hata juu kuliko wa leo, hatua kwa hatua ukikwea hata juu zaidi. Hii ndiyo kazi anayotumia Mungu kumkamilisha mwanadamu. Iwapo mwanadamu hawezi kwenda sambamba, basi anaweza kuachwa nyuma wakati wowote. Kama mwanadamu hana moyo wa kutii, basi hawezi kufuata hadi mwisho. Enzi ya kale imepita; hii ni enzi mpya. Na katika enzi mpya, kazi mpya lazima ifanywe. Hasa katika enzi ya mwisho ambapo mwanadamu atakamilishwa, Mungu atafanya kazi mpya hata haraka zaidi. Hivyo, bila utii moyoni mwake, mwanadamu ataona vigumu kufuata nyayo za Mungu. Mungu hafuati kanuni zozote, wala hachukulii hatua yoyote ya kazi Yake kama isiyobadilika. Badala yake, kazi Anayofanya daima ni mpya zaidi na daima ni juu zaidi. Kazi Yake inazidi kuwa ya utendaji kwa kila hatua, sambamba zaidi na matendo halisi ya mwanadamu. Baada tu ya mwanadamu kuwa na uzoefu wa aina hii ya kazi ndipo anaweza kufikia mabadiliko ya mwisho ya tabia yake. Maarifa ya mwanadamu ya maisha yanakua hata juu zaidi, na vivyo hivyo kazi ya Mungu pia inakuwa juu zaidi. Mwanadamu anaweza kufikia ukamilifu kwa njia hii tu na kufaa kwa matumizi ya Mungu. Kwa upande mmoja, Mungu anafanya kazi hivi ili kupinga na kubadilisha fikira za mwanadamu,

na kwa upande mwingine, kumwongoza mwanadamu katika hali ya juu zaidi na kweli zaidi, hadi katika ulimwengu wa juu zaidi wa imani katika Mungu, ili mwishowe, mapenzi ya Mungu yaweze kufanyika. Wote walio na asili isiyotii wanaopinga kwa kusudi wataachwa nyuma na hatua hii ya kazi ya Mungu ya haraka na yenye kusonga mbele kwa nguvu; wale tu walio na moyo mtiifu na wako tayari kuwa wanyonge wataendelea hadi mwisho wa njia. Katika kazi kama hii, nyote mnapaswa kujua jinsi ya kutii na kuweka kando fikira zenu. Mnapaswa kuwa waangalifu katika kila hatua mnayochukua. Kama wewe ni mzembe, hakika utakuwa mmoja wa wale wanaochukiwa na kukataliwa na Roho Mtakatifu na yule anayemkatiza Mungu katika kazi Yake. Kabla ya kufanyiwa hatua hii ya kazi, kanuni na sheria za mwanadamu za zamani zilikuwa nyingi sana hadi akawa na msisimko zaidi, na mwishowe, akawa mwenye majivuno na kujisahau. Hivi vyote ni vikwazo vinavyomzuia mwanadamu kuikubali kazi mpya ya Mungu; vinakuwa pingamizi kwa mwanadamu kuja kumjua Mungu. Iwapo mwanadamu hana utii katika moyo wake wala tamaa ya ukweli, basi atakuwa hatarini. Ukitii tu kazi na maneno yaliyo rahisi, na huwezi kukubali yoyote yaliyo na ugumu zaidi, basi wewe ni yule anayeendelea na njia za zamani na hawezi kwenda sambamba na kazi ya Roho Mtakatifu. Kazi inayofanywa na Mungu ni tofauti kutoka kipindi kimoja hadi kingine. Ukionyesha utii mkubwa katika awamu moja, lakini katika awamu ifuatayo uonyeshe utii mdogo ama usionyeshe wowote, basi Mungu atakuacha. Ukienda sambamba na Mungu anapopaa hatua hii, basi lazima uendeleo kuwa sambamba Anapopaa ifuatayo. Ni hapo tu ndipo utakuwa mtu ambaye ni mtiifu kwa Roho Mtakatifu. Kwa sababu unamwamini Mungu, lazima ubakie daima katika utii wako. Huwezi tu kutii unapotaka na kutotii usipotaka. Namna hii ya utii haikubaliki na Mungu. Kama huwezi kwenda sambamba na kazi mpya Ninayoshiriki na uendeleo kuyashikilia maneno ya zamani, basi kutakuaje na ukuaji katika maisha yako? Kazi ya Mungu ni kukuruzuku kupitia neno Lake. Unapotii na kulikubali neno Lake, basi Roho Mtakatifu hakika atafanya kazi ndani yako. Roho Mtakatifu anafanya kazi kwa njia Ninayozungumza kabisa. Fanya Niliyosema, na Roho Mtakatifu atafanya kazi ndani yako mara moja. Natoa mwangaza mpya ili muweze kuona na kuwaleta kwa mwangaza wa wakati wa sasa. Unapotembea katika mwangaza huu, Roho Mtakatifu ataanza kazi ndani yako mara moja. Kuna wengine wanaoweza kuwa wakaidi na kusema, “Sitafanya tu Usemavyo.” Basi Nakwambia kwamba sasa umefika mwisho wa njia umenyauka na huna maisha zaidi. Hivyo, kwa kupitia mabadiliko ya tabia yako, ni muhimu kabisa kwenda sambamba na mwangaza wa sasa. Roho Mtakatifu hafanyi kazi tu kwa baadhi ya wanadamu wanaotumiwa na Mungu, lakini hata zaidi kanisani. Anaweza kuwa akifanya kazi kwa yeyote. Anaweza kufanya kazi ndani yako sasa, na baada ya wewe kuwa na uzoefu nayo, Anaweza kufanya kazi ndani ya mtu mwingine ajaye. Fanya hima ufuate; unapozidi kufuata mwangaza wa sasa, ndivyo maisha yako yanaweza ku kua. Haijalishi yeye ni mwanadamu wa aina gani, alimradi Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani yake, kuwa na hakika kufuata. Chukua

uzoefu wake kupitia wako mwenyewe, na utapokea mambo ya juu hata zaidi. Kwa kufanya hivyo utaona ukuaji haraka zaidi. Hii ni njia ya ukamilifu kwa mwanadamu na njia ambayo maisha hukua. Njia ya ukamilifu inafikiwa kupitia utii wako wa kazi ya Roho Mtakatifu. Hujui ni kupitia kwa mtu wa aina gani ndiyo Mungu Atafanya kazi kukukamilisha, wala kupitia mtu yupi, tukio, ama jambo ndiyo Atakuwezesha kuingia katika umiliki na kupata ufahamu fulani. Ukiweza kutembea kwenye njia hii sawa, hii inaonyesha kwamba kuna matumaini makubwa kwako kukamilishwa na Mungu. Kama huwezi kufanya hivyo, inaonyesha kwamba maisha yako ya baadaye ni ya dhalili na giza. Mara unapoenda kwenye njia iliyo sahihi, utapata ufunuo katika mambo yote. Bila kujali yale ambayo Roho Mtakatifu atafichua kwa wengine, ukiendelea kupitia mambo wewe mwenyewe kwa msingi wa maarifa yao, basi uzoefu huu utakuwa sehemu ya maisha yako, na utaweza kuwakimu wengine kwa sababu ya huu uzoefu. Wale wanaowakimu wengine kwa kuyarudia maneno ni wale wasio na uzoefu wowote; lazima ujifunze kupata, kupitia mwangaza na nuru ya wengine, njia ya kutenda kabla ya kuzungumza kuhusu uzoefu na maarifa yako halisi. Hii itakuwa ya manufaa zaidi kwa maisha yako binafsi. Unapaswa kuwa na uzoefu kwa njia hii, kutii yote yatokayo kwa Mungu. Unapaswa kutafuta mapenzi ya Mungu katika vitu vyote na kujifunza masomo katika vitu vyote, ili maisha yako yaweze kukua. Vitendo vya aina hii huleta ukuaji wa haraka zaidi.

Roho Mtakatifu anakupa nuru kupitia uzoefu wa vitendo vyako na kukukamilisha kupitia imani yako. Uko tayari kweli kukamilishwa? Kama kweli uko tayari kukamilishwa na Mungu, basi utakuwa na ujasiri kuweka kando mwili wako, na utaweza kutekeleza maneno ya Mungu na kutokuwa mtu anayekaa tu ama mnyonge. Utaweza kutii yote yatokayo kwa Mungu, na vitendo vyako vyote, viwe vimefanywa hadharani au faraghani, vitastahiki kwa Mungu. Kama wewe ni mtu mwaminifu, na unatenda ukweli katika mambo yote, basi utakamilishwa. Wale wanadamu wadanganyifu wanaotenda njia moja mbele ya wengine na nyingine nyuma yao hawako tayari kukamilishwa. Wote ni wana wa maangamizo na uharibifu; wao si wa Mungu lakini ni wa Shetani. Hao si aina ya wanadamu waliochaguliwa na Mungu! Kama vitendo na tabia yako haviwezi kustahiki mbele ya Mungu ama kufikiriwa na Roho wa Mungu, hii ni thibitisho kwamba wewe una shida. Ukikubali tu hukumu na kuadibu kwa Mungu, na kuweka umuhimu katika mabadiliko ya tabia yako ndipo utafika kwenye njia ya kukamilishwa. Ikiwa kweli uko tayari kukamilishwa na Mungu na kufanya mapenzi ya Mungu, basi unapaswa kutii kazi yote ya Mungu na kutotoa neno lolote la kulalamika, wala hupaswi kutathmini ama kuhukumu kazi ya Mungu utakavyo. Haya ni masharti ya msingi kabisa ya kukamilishwa na Mungu. Mahitaji ya lazima kwa wale wanaotaka kukamilishwa na Mungu ni haya: fanya mambo yote kwa moyo unaompenda Mungu. Inamaanisha nini “kufanya mambo kwa moyo unaompenda Mungu”? Inamaanisha kwamba vitendo na tabia yako yote inaweza kuletwa mbele ya Mungu. Kwa sababu

una nia sawa, iwapo vitendo vyako ni sawa ama vibaya, huogopi vikionyeshwa kwa Mungu ama kwa ndugu zako; unathubutu kuapa mbele ya Mungu. Lazime uonyeshe kila nia, fikra, na wazo lako mbele ya Mungu ili ayachunguze; ukitenda na kuingia kwa njia hii, basi maendeleo katika maisha yako yatakuwa mepesi.

Kwa sababu unamwamini Mungu, basi lazima uweke imani ndani ya maneno yote ya Mungu na ndani ya kazi Yake yote. Hii ni kusema kwamba, kwa sababu unamwamini Mungu, ni lazima umtii. Kama huwezi kufanya hivi, basi haijalishi iwapo unamwamini Mungu. Kama umemwamini Mungu kwa miaka mingi, lakini hujawahi kumtii ama kuyakubali maneno Yake, na badala yake umemwuliza Mungu anyenyekee kwako na kufuata dhana zako, basi wewe ni mtu mwasi zaidi ya wote, na wewe si muumini. Mtu kama huyu anawezaje kutii kazi na maneno ya Mungu ambayo hayafuati fikira za mwanadamu? Mtu mwasi zaidi ni yule anayemkataa na kumpinga Mungu makusudi. Yeye ni adui wa Mungu na ni mpinga Kristo. Mtu kama huyu daima anakuwa na mtazamo wa kikatili kwa kazi mpya ya Mungu, hajawahi kuonyesha nia hata ndogo ya kutii, na hajawahi kuonyesha utii ama kujinyenyekeza kwa furaha. Anajisifu mbele ya wengine na kamwe haonyeshi utii kwa mwingine. Mbele ya Mungu, anajiona kuwa hodari zaidi katika kuhubiri neno na mwenye ujuzi zaidi katika kufanya kazi kwa wengine. Kamwe hatupi “hazina” anazomiliki tayari, lakini anazichukua kama vitu vinavyorithiwa kwa familia vya kuabudiwa, vya kuhubiri kuhusu wengine, na huvitumia kuhutubia wale wapumbavu wanaomwabudu. Hakika kuna baadhi ya watu kama hawa kanisani. Inaweza kusemwa kwamba wao ni “mashujaa wasioshindwa,” kizazi baada ya kizazi kinachokaa kwa muda mfupi ndani ya nyumba ya Mungu. Wanachukua kuhubiri neno (mafundisho ya dini) kama wajibu wao wa juu zaidi. Mwaka baada ya mwaka na kizazi baada ya kizazi, wao huenenda kwa nguvu wakitekeleza wajibu wao “mtakatifu na usiokiukwa”. Hakuna anayethubutu kuwaguzi na hakuna mtu hata mmoja anayethubutu kuwashutumu kwa uwazi. Wanakuwa “wafalme” katika nyumba ya Mungu, wakienea kote wakiwaonea wengine kutoka enzi hadi enzi. Hili kundi la mapepo linataka kuungana mikono na kuharibu kazi Yangu; Naweza kuwaruhusu ibilisi hawa waishio kuwepo mbele Yangu? Hata wale walio tu na moyo nusu wa utii hawawezi kutembea hadi mwisho, sembuse hawa wadhalimu wasio na utii hata kidogo kwa mioyo yao. Kazi ya Mungu haipatwi virahisi na mwanadamu. Hata mwanadamu akitumia nguvu yake yote, ataweza kupata kipande tu na kufikia ukamilifu mwishowe. Na vipi basi kuhusu watoto wa malaika mkuu wanaotaka kuharibu kazi ya Mungu? Je, hawana hata matumaini madogo zaidi ya kupatwa na Mungu? Madhumuni Yangu katika kufanya kazi ya ushindi si tu kushinda kwa sababu ya ushindi, lakini kushinda ili kufichua haki na udhalimu, kupata ushahidi kwa ajili ya adhabu ya mwanadamu, kulaani waovu, na hata zaidi, kushinda kwa sababu ya kuwakamilisha wale walio radhi kutii. Mwishowe, wote watatengwa kulingana na aina, na mawazo ya wale wote

waliokamilishwa yatajazwa na utii. Hii ndiyo kazi itakayokamilishwa mwishowe. Lakini waliojawa na uasi wataadhibiwa, kutumwa kuchomeka motoni na milele kulaaniwa. Wakati huo utakapofika, wale “mashujaa wakubwa wasioshindwa” wa awali watakuwa “waoga wanyonge na wasio na maana” wa chini zaidi na wanaoepukwa zaidi. Hii tu ndiyo inaweza kuonyesha kila kipengele cha haki ya Mungu na kufichua tabia Yake ambayo hairuhusu kosa lolote. Hili tu ndilo linaloweza kutuliza chuki iliyo moyoni Mwangu. Je, hamkubali kwamba hili ni la busara sana?

Sio wote walio na uzoefu wa kazi ya Roho Mtakatifu wanaweza kupata uzima, na sio wote katika mkondo huu wanaweza kupata uzima. Uzima sio mali ya kawaida inayoshirikisha binadamu wote, na mabadiliko ya tabia ni kitu ambacho hakifikiwi na wote kwa urahisi. Kujisalimisha kwa kazi ya Mungu lazima kugusike na kuishi kwa kudhihirishwa. Kujisalimisha kwa kiwango cha juu juu hakuwezi kupokea idhini ya Mungu, na kutii tu vipengele vya juujuu vya neno la Mungu bila kutaka mgeuzo wa tabia ya mtu, hakutaweza kuufurahisha moyo wa Mungu. Utiifu kwa Mungu na kujinyenyekeza kwa kazi ya Mungu ni kitu kimoja. Wale wanaomtii Mungu tu lakini hawatii kazi Yake hawawezi kudhaniwa kuwa watiifu, sembuse wale wasiotii kwa kweli na kwa nje hao ni wa kujipendekeza. Wale ambao kweli wanajinyenyekeza kwa Mungu wote wanaweza kufaidika kutokana na kazi na kupata ufahamu wa tabia na kazi ya Mungu. Wanadamu kama hawa tu ndio kweli wanajinyenyekeza kwa Mungu. Wanadamu kama hawa wanaweza kupata maarifa mapya kutokana na kazi mpya na kuwa na uzoefu wa mabadiliko mapya kutoka hayo. Wanadamu kama hawa tu ndio wana idhini ya Mungu; mwanadamu wa aina hii tu ndiye amekamilishwa, ndiye amepitia mabadiliko ya tabia yake. Wale wanaopokea idhini ya Mungu ni wale wanaojisalimisha kwa Mungu kwa furaha, na pia kwa neno na kazi Yake. Mwanadamu wa aina hii tu ndiye yuko sahihi; mwanadamu wa aina hii tu ndiye kweli anamtamani Mungu, na anamtafuta Mungu kwa dhati. Na kwa wale wanaozungumzia tu imani yao kwa Mungu kwa vinywa vyao lakini kwa hakika wanamlaani, ni wanadamu waliovaa barakoa, walio na sumu ya nyoka, ni wanadamu wasaliti zaidi. Siku moja hawa waovu watavuliwa barakoa zao mbovu. Je, hiyo si kazi inayofanywa leo? Wanadamu waovu daima watakuwa waovu na hawataepuka kamwe siku ya adhabu. Wanadamu wazuri daima watakuwa wazuri na watafichuliwa kazi itakapoisha. Hakuna hata mmoja wa waovu atakayedhaniwa kuwa wenye haki, wala yeyote mwenye haki atakayedhaniwa kuwa mwovu. Je, Ningemruhusu yeyote ashtakiwe kimakosa?

Maisha yako yanapoendelea, lazima daima uwe na kiingilio kipyaa na ufahamu mpya na wa juu zaidi, unaokua kwa kina na kila hatua. Hiki ndicho wanadamu wote wanapaswa kuingia ndani. Kupitia kuwasiliana, kusikiliza ujumbe, kusoma neno la Mungu, ama kushughulikia suala, utapata ufahamu mpya na kupata nuru upya. Huishi ndani ya kanuni za zamani na nyakati za zamani. Unaishi daima ndani ya mwangaza mpya, na hupotei mbali na neno la Mungu. Huku

ndiko kunaitwa kwenda katika njia sahihi. Kulipa tu gharama ya juu juu hakutakubalika. Siku baada ya siku, neno la Mungu linaingia katika ulimwengu wa juu zaidi na mambo mapya yanajitokeza kila siku. Ni muhimu pia kwa mwanadamu kuingia upya kila siku. Mungu anavyozungumza, ndivyo Anavyotimiza yote ambayo Amezungumza; kama huwezi kwenda sambamba, basi unabaki nyuma. Lazima uende kwa kina zaidi katika maombi yako; kula na kunywa neno la Mungu hakuwezi kuwa kuna kosa mfululizo. Imarisha nuru na mwangaza unayopokea, ufunuo unaopokea, na dhana zako na fikira zako lazima zipungue hatua kwa hatua. Lazima pia uimarisha hekima yako, na chochote unachopitia, lazima uwe na mawazo yako kukihusu na uwe na mtazamo wako. Kwa kuelewa mambo fulani katika roho, lazima upate ufahamu wa mambo ya nje na kuelewa kiini cha suala lolote. Kama hujajiandaa na mambo haya, utawezaje kuliongoza kanisa? Iwapo unazungumzia tu barua na mafundisho ya dini bila uhalisi wowote na bila njia ya kutenda, unaweza tu kuendelea kwa muda mfupi. Inaweza kukubalika kidogo kwa waumini wapya, lakini baada ya muda, wakati waumini wapya wanapata tajriba halisi, basi hutaweza tena kuwakimu. Basi unafaa vipi kwa matumizi ya Mungu? Bila kupata nuru upya, huwezi kufanya kazi. Walio bila nuru upya ni wale wasiojua jinsi ya kuwa na uzoefu, na wanadamu kama hao kamwe hawapati maarifa mapya ama tajriba. Na katika suala la kuleta maisha, hawawezi kamwe kufanya jukumu lao la kusambaza uhai, wala hawawezi kufaa kwa ajili ya matumizi na Mungu. Mwanadamu kama huyu ni dhaifu na hana maana. Kwa kweli, wanadamu kama hawa hawawezi kufanya jukumu lao kabisa kwa kazi na wote hawana faida. Wanashindwa kufanya jukumu lao na pia kwa kweli wanaweka mzigo mwingi usiohitajika juu ya kanisa. Nawahimiza hawa “wanaume wazee” kuharakisha na kuondoka kanisani ili wengine wasilazimishwe kuwaona tena. Wanadamu kama hawa hawaelewi kazi mpya lakini wamejawa na fikira zisizokoma. Hawafanyi chochote kanisani; badala yake, wanachochea na kusambaza uhasi kila pahali, hata kushiriki katika kila namna ya utovu wa nidhamu na vurugu kanisani, na hivyo kuwarusha wale wasiobagua katika vurugu na machafuko. Haya ibilisi wanaoishi, hawa mapepo mabaya wanapaswa kuondoka kanisani haraka iwezekanavyo, kanisa lisije likaharibiwa kwa sababu yako. Labda huogopi kazi ya leo, lakini huogopi adhabu ya haki ya kesho? Kuna idadi kubwa ya watu kanisani ambao ni vimelea, na pia kuna idadi kubwa ya mbwa mwitu wanaotafuta kuvuruga kazi ya kawaida ya Mungu. Vitu hivi vyote ni mapepo yaliyotumwa na Ibilisi, ni mbwa mwitu wakali wanaotafuta kuwala kondoo wasiojua. Iwapo wanadamu kama hawa hawatafukuzwa, basi wanakuwa vimelea kwa kanisa na nondo wanaokula sadaka. Hawa mabuu wenye kudharauliwa wajinga, duni, na wenye kuchukiza wataadhibiwa siku moja karibuni!

Enzi ya Ufalme Ni Enzi ya Neno

Katika Enzi ya Ufalme, Mungu hutumia maneno kuikaribisha enzi mpya, kubadilisha njia

ambayo kwayo Yeye hufanya kazi, na kufanya kazi ya enzi nzima. Hii ndiyo kanuni ambayo kwayo Mungu hufanya kazi katika Enzi ya Neno. Alikuwa mwili ili Anene kutoka katika mitazamo tofauti, ili mwanadamu aweze kumwona Mungu kweli, ambaye ni Neno kuonekana katika mwili, na angeweza kuona hekima na ajabu Yake. Kazi kama hiyo inafanywa ili kufikia malengo ya kumshinda mwanadamu, kumkamilisha mwanadamu, na kumwondoa mwanadamu vyema zaidi, ambayo ndiyo maana ya kweli ya matumizi ya maneno kufanya kazi katika Enzi ya Neno. Kupitia katika maneno haya, watu huja kujua kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, kiini cha mwanadamu, na kile ambacho mwanadamu anapaswa kuingia katika. Kupitia katika maneno, kazi ambayo Mungu anataka kufanya katika Enzi ya Neno inafanikiwa kwa ukamilifu. Kupitia katika maneno haya, watu wanafunuliwa, kuondolewa, na kujaribiwa. Watu wameyaona maneno ya Mungu, kuyasikia maneno haya, na kutambua uwepo wa maneno haya. Kama matokeo, wameamini katika uwepo wa Mungu, katika kudura na hekima ya Mungu, na pia katika upendo wa Mungu kwa mwanadamu na tamanio Lake la kumwokoza mwanadamu. Neno "maneno" linaweza kuwa rahisi na la kawaida, lakini maneno yanayonenwa kutoka katika kinywa cha Mungu mwenye mwili yanautikisa ulimwengu, kuibadilisha mioyo ya watu, kubadilisha fikira zao na tabia zao za zamani, na kubadilisha jinsi ambavyo ulimwengu wote ulikuwa ukionekana. Katika enzi zote, ni Mungu wa leo tu ndiye Aliyefanya kazi kwa njia hii, na ni Yeye Anayezungumza kwa namna hii na kuja kumwokoza mwanadamu hivi. Kuanzia wakati huu na kuendelea, mwanadamu anaishi chini ya mwongozo wa maneno ya Mungu, akichungwa na kuruzukiwa na maneno Yake. Watu wanaishi katika ulimwengu wa maneno ya Mungu, kati ya laana na baraka za maneno ya Mungu, na kuna hata watu wengi zaidi ambao wamekuja kuishi chini ya hukumu na kuadibu kwa maneno Yake. Maneno haya na kazi hii vyote ni kwa sababu ya wokovu wa mwanadamu, kwa sababu ya kutimiza mapenzi ya Mungu, na kwa sababu ya kubadilisha kuonekana kwa asili kwa ulimwengu wa uumbaji wa zamani. Mungu aliuumba ulimwengu kwa kutumia maneno, Anawaongoza watu ulimwenguni kote kutumia maneno, na Anawashinda na kuwaokoa kutumia maneno. Hatimaye, Atatumia maneno kuutamatisha ulimwengu mzima wa zamani, hivyo kuukamilisha mpango Wake mzima wa usimamizi. Katika Enzi nzima ya Ufalme, Mungu hutumia maneno kufanya kazi Yake, na kufikia matokeo ya kazi Yake. Hatendi maajabu au kufanya miujiza, lakini hufanya kazi Yake kupitia katika maneno tu. Kwa sababu ya maneno haya, mwanadamu hulishwa na kuruzukiwa, na hupata maarifa na uzoefu wa kweli. Katika Enzi ya Neno, mwanadamu amebarikiwa kwa njia ya pekee. Hapitii uchungu wa mwili na hufurahia tu ruzuku nyingi ya maneno ya Mungu; bila kuhitaji kwenda kutafuta bila kufikiri au kusafiri mbele bila kufikiri, kutoka katikati ya utulivu wake, huiona sura ya Mungu, humsikia Akinena kwa kinywa Chake mwenyewe, hupokea kile ambacho Yeye hutoa, na humtazama Akifanya kazi Yake binafsi. Hivi ni vitu ambavyo watu wa enzi zilizopita hawakuweza kufurahia, na ni baraka ambazo hawangeweza kupokea kamwe.

Mungu ameamua kumfanya mwanadamu mkamilifu, na bila kujali mtazamo ambao Ananena kutoka, yote ni kwa sababu ya kuwafanya watu wawe wakamilifu. Maneno yanenwayo kutoka katika mtazamo wa Roho ni magumu kwa watu kuelewa; hawana namna ya kupata njia ya kutenda, kwa kuwa uwezo wao wa kuelewa ni finyu. Kazi ya Mungu inafikia matokeo tofauti, na katika kuchukua kila hatua ya kazi Ana kusudi Lake. Aidha, ni muhimu kwamba Azungumze kutoka katika mitazamo tofauti, kwa kuwa ni kwa kufanya hivyo tu ndipo Anaweza kumkamilisha mwanadamu. Kama Angetamka sauti Yake kutoka katika mtazamo wa Roho tu, hakungekuwa na njia yoyote ya kukamilisha hatua hii ya kazi ya Mungu. Kutoka katika sauti Anayozungumza nayo, unaweza kuona kwamba Amedhamiria kulifanya kundi hili la watu kamilifu. Kwa hivyo, hatua ya kwanza kwa kila anayetamani kukamilishwa inapasa kuwa ipi? Zaidi ya yote, lazima ujue kazi ya Mungu. Leo, njia mpya imeanza katika kazi ya Mungu; enzi imebadilika, namna ambavyo Mungu hufanya kazi pia imebadilika, na njia ambayo Mungu huzungumza ni tofauti. Leo, sio tu kwamba njia ya kazi Yake imebadilika, lakini pia enzi imebadilika. Sasa ni Enzi ya Ufalme. Pia ni Enzi ya kumpenda Mungu. Ni kionjo cha Enzi ya Ufalme wa Milenia—ambayo pia ni Enzi ya Neno, na ambayo Mungu hutumia njia nyingi za kunena ili kumkamilisha mwanadamu, na Ananena kutoka katika mitazamo tofauti ili kumruzuku mwanadamu. Baada ya kuingia katika Enzi ya Ufalme wa Milenia, Mungu ataanza kutumia maneno kumfanya mwanadamu awe mkamilifu, Akimruhusu mwanadamu aingie katika uhalisi wa maisha na kumwongoza kwenye njia sahihi. Mwanadamu amepitia hatua nyingi sana za kazi Yake na ameona kuwa kazi ya Mungu haibaki vile vile, lakini inageuka na kuongezeka kwa kina bila kukoma. Baada ya watu kuipitia kwa muda mrefu sana, kazi imebadilika kwa kurudia rudia, ikibadilika tena na tena. Hata hivyo, bila kujali kiasi inachobadilika, kamwe haikengeuki kutoka kwa kusudi la Mungu la kuwaletea binadamu wokovu. Hata kupitia katika mabadiliko elfu kumi, kamwe haipotei kutoka kwa kusudi lake la asili. Bila kujali jinsi mbinu ya kazi ya Mungu inavyoweza kubadilika, kazi hii kamwe haiuachi ukweli au uzima. Mabadiliko katika njia ambayo kazi hufanywa inahusisha mabadiliko katika muundo wa kazi tu, na mtazamo ambao kwao Mungu ananena; hakuna mabadiliko katika kusudi kuu la kazi ya Mungu. Mabadiliko katika toni ya sauti ya Mungu na njia ya kazi Yake hufanywa ili kufikia matokeo. Mabadiliko katika toni ya sauti hayamaanishi mabadiliko katika madhumuni au kanuni ya kazi hiyo. Watu wanamwamini Mungu hasa ili kutafuta uzima; ikiwa unaamini katika Mungu lakini hutafuti uzima au hufuatilii ukweli au maarifa ya Mungu, basi hii siyo imani katika Mungu! Na, je, bado ni jambo lenye uhalisi kutafuta kuingia katika ufalme kuwa mfalme? Kufanikisha upendo wa kweli kwa Mungu kupitia kutafuta uzima—huu pekee ndio uhalisi; ufuatiliaji na utendaji wa ukweli—hivi vyote ni uhalisi. Kusoma maneno ya Mungu, na kuyapitia maneno haya, utakuja kufahamu maarifa ya Mungu katika uzoefu halisi, na hii ndiyo maana ya kufuatilia kweli.

Sasa ni Enzi ya Ufalme. Ikiwa umeingia katika enzi hii mpya inategemea ikiwa umeingia katika uhalisi wa maneno ya Mungu, ikiwa maneno Yake yamekuwa uhalisi wa maisha yako. Maneno ya Mungu yanafahamishwa kwa kila mtu ili, mwishowe, watu wote wataishi katika ulimwengu wa maneno ya Mungu, na maneno Yake yatampa nuru na kumwaganzia kila mtu kutoka ndani. Ikiwa, wakati huu, wewe ni mzembe katika kusoma maneno ya Mungu, na huna shauku ya maneno Yake, basi hili linaonyesha kuwa hali yako ni mbaya. Ikiwa huwezi kuingia katika Enzi ya Neno, basi Roho Mtakatifu hafanyi kazi ndani yako; ikiwa umeingia katika enzi hii, Atafanya kazi Yake. Je, unaweza kufanya nini mwanzoni mwa Enzi ya Neno ili upate kazi ya Roho Mtakatifu? Katika enzi hii, na miongoni mwenu, Mungu atatimiza ukweli ufuatao: kwamba kila mtu ataishi kwa kuyadhihirisha maneno ya Mungu, ataweza kuuweka ukweli katika vitendo, na atampenda Mungu kwa dhati; kwamba watu wote watatumia maneno ya Mungu kama msingi na kama uhalisi wao, na watakuwa na mioyo inayomcha Mungu; na kwamba, kupitia kutenda maneno ya Mungu, mwanadamu kisha atashikilia mamlaka ya kifalme pamoja na Mungu. Hii ndiyo kazi inayopaswa kufanikishwa na Mungu. Je, unaweza kuishi bila kusoma maneno ya Mungu? Leo, kuna wengi ambao wanahisi kuwa hawawezi kuishi hata siku moja au mbili bila kusoma maneno Yake. Lazima wayasome maneno Yake kila siku, na ikiwa muda hauruhusu, kuyasikiza kutatosha. Hii ndiyo hisia ambayo Roho Mtakatifu huwapa watu, na ndiyo njia ambayo Anaanza kuwagusa. Yaani, Yeye huwatawala watu kupitia maneno, ili kwamba waweze kuingia katika uhalisi wa maneno ya Mungu. Ikiwa, baada ya siku moja tu bila kula na kunywa maneno ya Mungu, unahisi giza na kiu, na huwezi kustahimili hali hiyo, hili linaonyesha kwamba umeguswa na Roho Mtakatifu, na kwamba Hajakukuacha. Wewe basi, ni mtu aliye kwenye mkondo huu. Hata hivyo, ikiwa baada ya siku moja au mbili bila kula na kunywa maneno ya Mungu, huhisi kitu, ikiwa huna kiu, na hujaguswa hata kidogo, hili linaonyesha kwamba Roho Mtakatifu amekuacha. Hili linamaanisha, basi, kwamba kuna kitu kibaya na hali yako; hujaingia katika Enzi ya Neno, na wewe ni mmoja wa wale ambao wamebaki nyuma. Mungu hutumia maneno kuwatawala watu; unahisi vizuri ukila na kunywa maneno ya Mungu, na usipokula na kunywa maneno ya Mungu, huna njia ya kufuata. Maneno ya Mungu huwa chakula cha watu, na nguvu inayowaendesha. Biblia inasema “Mwanadamu hataishi kwa mkate pekee, lakini kwa kila neno linalotoka kinywani mwa Mungu”. Leo, Mungu ataikamilisha kazi hii, naye Ataukamilisha ukweli huu ndani yenu. Ni vipi kwamba hapo zamani, watu wangeweza kwenda siku nyingi bila kusoma maneno ya Mungu na bado waweze kula na kufanya kazi kama kawaida, lakini hivi sivyo ilivyo leo? Katika enzi hii, Mungu haswa hutumia maneno kutawala vyote. Kupitia katika maneno ya Mungu, mwanadamu anahukumikiwa na kukamilishwa, kisha hatimaye kupelekwa katika ufalme. Maneno ya Mungu tu ndiyo yanayoweza kuyaruzuku maisha ya mwanadamu, na ni maneno ya Mungu tu yanayoweza kumpa mwanadamu mwangaza na njia ya kutenda, hasa katika Enzi ya Ufalme. Alimradi hupotei

kutoka katika ukweli wa maneno ya Mungu, kula na kunywa maneno Yake kila siku, Mungu ataweza kukufanya mkamilifu.

Ufuatiliaji wa maisha si jambo ambalo linaweza kuharakishwa; ukuaji wa maisha haufanyiki kwa siku moja au mbili. Kazi ya Mungu ni ya kawaida na ya vitendo, na kuna mchakato ambao lazima ipitie. Ilimchukua Yesu mwenye mwili miaka thelathini na mitatu na nusu kukamilisha kazi Yake ya kusulubiwa—sembuse kazi ya kumtakasa mwanadamu na kuyabadilisha maisha yake, kazi ngumu zaidi? Sio kazi rahisi kumfanya mwanadamu wa kawaida ambaye anamdhihirisha Mungu. Hili ni hivyo hasa kwa watu ambao wamezaliwa katika taifa la joka kubwa jekundu, ambao ni wenye ubora duni wa tabia na wanahitaji muda mrefu wa maneno na kazi ya Mungu. Kwa hivyo usiwe bila subira kutaka kuona matokeo. Lazima uwe mwenye kujitolea katika kula na kunywa maneno ya Mungu, na uweke bidii zaidi katika maneno ya Mungu. Unapomaliza kusoma maneno Yake, lazima uweze kuyaweka katika vitendo halisi, ukikua katika maarifa, ufahamu, utambuzi, na hekima katika maneno ya Mungu. Kupitia katika hili, utabadilika bila kufahamu. Ikiwa unaweza kuchukua kula na kunywa maneno ya Mungu kama kanuni yako, ukiyasoma, ukija kuyajua, kuyapitia, na kuyatenda, utakuwa mkomavu bila kufahamu. Kuna wale ambao wanasema kuwa hawawezi kuyaweka maneno ya Mungu katika vitendo hata baada ya kuyasoma. Haraka yako ni nini? Utakapofikia kimo fulani, utaweza kuyaweka maneno Yake katika vitendo. Je, mtoto wa umri wa miaka minne au mitano anaweza kusema kuwa hawezi kuwasaidia au kuwaheshimu wazazi wake? Unapaswa kujua jinsi kimo chako cha sasa kilivyo kikubwa. Weka katika vitendo kile unachoweza kuweka katika vitendo, na uepukane na kuwa mtu ambaye anasumbua usimamizi wa Mungu. Kula na kunywa maneno ya Mungu tu, na ulichukue hilo kama kanuni yako kuanzia sasa kuendelea. Usijali, kwa wakati huu, kuhusu ikiwa Mungu anaweza kukufanya mkamilifu. Usilichunguze hilo kwa sasa. Kula na kunywa maneno ya Mungu tu yanavyokujia, na Mungu hakika Atakufanya mkamilifu. Hata hivyo, kuna kanuni ambayo kwayo lazima ule na kunywa maneno Yake. Usifanye hivyo tu bila kufikiria. Katika kula na kunywa maneno ya Mungu, kwa upande mmoja, yatafute maneno ambayo unapaswa kuyajua—yaani, yale yanayohusiana na maono—na kwa upande mwingine, tafuta kile unachopaswa kuweka katika vitendo halisi—yaani, kile unachopaswa kuingia ndani. Kipengele kimoja kinahusiana na maarifa, na kingine kinahusiana na kuingia. Mara unapovifahamu vyote viwili—wakati umeshaelewa kile unachopaswa kujua na kile unachopaswa kutenda utajua jinsi ya kula na kunywa maneno ya Mungu.

Kuanzia sasa kuendela, mazungumzo ya maneno ya Mungu yanapaswa kuwa kanuni ambayo kwayo unazungumza. Kwa kawaida, mnajumuika pamoja, mnapaswa kushiriki katika ushirika kuhusu maneno ya Mungu, mkiyachukua maneno ya Mungu kama maudhui ya mwingiliano wenu, mkiongea juu ya yale mnayojua kuhusu maneno haya, jinsi mnavyoyaweka

katika vitendo, na jinsi Roho Mtakatifu afanyavyo kazi. Alimradi unashiriki maneno ya Mungu, Roho Mtakatifu atakupa nuru. Kufanikisha ulimwengu wa maneno ya Mungu kunahitaji ushirikiano wa mwanadamu. Usipoingia katika hili, Mungu hatakuwa na njia ya kufanya kazi; ukiufunga mdomo wako na usizungumze kuhusu maneno Yake, Hatakuwa na njia ya kukuangazia. Wakati wowote ambapo huna shughuli nyingine, zungumza juu ya maneno ya Mungu, na usijishughulisha na mazungumzo yasiyo na maana! Acha maisha yako yajazwe na maneno ya Mungu—ni hapo tu ndipo utakapokuwa mwumini mwenye kumcha Mungu. Haijalishi ikiwa ushirika wako ni wa juu juu. Bila ujuu juu hakuwezi kuwepo kina kirefu. Lazima kuwe na mchakato. Kupitia mafunzo yako, utafahamu kuangaziwa kwako na Roho Mtakatifu, na jinsi ya kula na kunywa maneno ya Mungu kwa matokeo yanayotarajiwa. Baada ya muda wa uchunguzi, utaingia katika ukweli wa maneno ya Mungu. Ni ukiamua kushirikiana tu ndipo utaweza kupokea kazi ya Roho Mtakatifu.

Kati ya kanuni za kula na kunywa maneno ya Mungu, moja inahusiana na maarifa, na nyingine inahusiana na kuingia. Ni maneno yapi unayopaswa kujua? Unapaswa kujua maneno yanayohusiana na maono (kama vile, yale yanayohusiana na ni enzi ipi ambayo kazi ya Mungu imeingia sasa, kile ambacho Mungu anataka kufanikisha sasa, kupata mwili ni nini, na kadhalika; haya yote yanahusiana na maono). Je, njia ambayo mwanadamu anapaswa kuingia katika inamaanisha nini? Hii inahusu maneno ya Mungu ambayo mwanadamu anapaswa kutenda na kuingia ndani. Yaliyo hapo juu ni vipengele viwili vya kula na kunywa maneno ya Mungu. Kuanzia sasa, kula na kunywa maneno ya Mungu kwa njia hii. Ukiwa na ufahamu wazi wa maneno Yake kuhusu maono, basi hakuna haja ya kuendelea kusoma kila wakati. Jambo la umuhimu wa msingi ni kula na kunywa maneno zaidi ya kuingia, kama vile kuugeza moyo wako kwa Mungu, jinsi ya kuutuliza moyo wako mbele za Mungu, na jinsi ya kuunyima mwili. Hivi ni vitu ambavyo unapaswa kuweka katika vitendo. Bila kujua jinsi ya kula na kunywa maneno ya Mungu, ushirika wa kweli hauwezekani. Mara tu unapojua jinsi ya kula na kunywa maneno Yake, wakati ambapo umeelewa kile kilicho muhimu, ushirika utakuwa wazi, na suala lolote liibuliwalo, utaweza kushirikiana na kufahamu uhalisi. Ikiwa, wakati unashiriki kuhusu maneno ya Mungu, huna uhalisi wowote, basi hujaelewa kile kilicho cha muhimu, ambalo linaonyesha kuwa hujui jinsi ya kula na kunywa maneno ya Mungu. Watu wengine wanaweza kupata kusoma maneno ya Mungu kuwa jambo la kuchosha, ambayo sio hali ya kawaida. Kilicho cha kawaida ni kamwe kutochoka kuyasoma maneno ya Mungu, kuwa na kiu ya maneno hayo kila wakati, na daima kuyaona maneno ya Mungu kuwa mazuri. Hivi ndivyo mtu ambaye ameingia kwa kweli hula na kunywa maneno ya Mungu. Unapohisi kuwa maneno ya Mungu ni ya vitendo sana na ndiyo mwanadamu anapaswa kuingia katika hasa; unapohisi kuwa maneno Yake ni ya msaada mkubwa na yenye faida kwa mwanadamu, na kwamba ni riziki ya maisha ya

mwanadamu—ni Roho Mtakatifu anayekupa hisia hii, na Roho Mtakatifu anayekugusa. Hii inathibitisha kuwa Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani yako na kwamba Mungu hajakuacha. Watu wengine, wakiona kuwa Mungu huzungumza kila wakati, huchoka na maneno Yake, na hufikiria kwamba haina athari wakiyasoma au la—ambayo si hali ya kawaida. Wanakosa moyo ambao unatamani kuingia katika uhalisi, na watu kama hao hawana kiu wala hawaoni umuhimu wa kukamilishwa. Kila unapopata kuwa huna kiu ya maneno ya Mungu, hii inaonyesha kuwa hauko katika hali ya kawaida. Hapo zamani, ikiwa Mungu angekuwa Amekuacha kungeweza kuamuliwa na ikiwa ulikuwa na amani ndani yako, na ikiwa uliona furaha. Sasa cha muhimu ni ikiwa una kiu ya maneno ya Mungu, ikiwa maneno Yake ni uhalisi wako, ikiwa wewe ni mwaminifu, na ikiwa unaweza kumfanyia Mungu yote uwezayo. Kwa maneno mengine, mwanadamu anahukumiwa na uhalisi wa maneno ya Mungu. Mungu huelekeza maneno Yake kwa binadamu wote. Ikiwa uko tayari kuyasoma, Atakupa nuru, lakini ikiwa hauko tayari, Hatafanya hivyo. Mungu huwapa nuru wale ambao wana njaa na kiu ya haki, na Huwapa nuru wale wanaomtafuta. Wengine husema kwamba Mungu hakuwapa nuru hata baada ya kusoma maneno Yake. Lakini uliyasoma maneno haya kwa njia gani? Ukiyasoma maneno Yake kama ambavyo mtu asiye ba shauku, na usiweke umuhimu katika uhalisi, Mungu angeweza kukupa nuru? Mtu ambaye hayathamini maneno ya Mungu anawezaje kufanywa mkamilifu na Yeye? Ikiwa huyathamini maneno ya Mungu, basi hutakuwa na uhalisi wala ukweli. Ikiwa unayathamini maneno Yake, basi utaweza kuuweka ukweli katika vitendo, na ni hapo tu ndipo utakapomiliki uhalisi. Hii ndiyo maana lazima ule na kunywa maneno ya Mungu wakati wote, iwe una shughuli nyingi au la, hali iwe mbaya au la, na iwe unajaribiwa au la. Kwa jumla, maneno ya Mungu ndiyo msingi wa kuwepo kwa mwanadamu. Hakuna anayeweza kuyaepuka maneno Yake, lakini lazima ale maneno Yake kama anavyokula milo mitatu ya siku. Je, kufanywa mkamilifu na kupatwa na Mungu kunaweza kuwa rahisi vile? Ikiwa wewe unaelewa kwa sasa au la, na ikiwa una utambuzi juu ya kazi ya Mungu au la, lazima ule na kunywa maneno mengi ya Mungu iwezekanavyo. Huku ni kuingia kwa njia ya vitendo. Baada ya kusoma maneno ya Mungu, harakisha kutia katika vitendo kile unachoweza kuingia katika, na uweke kando kwa sasa kile ambacho huwezi. Kunaweza kuwa na maneno mengi ya Mungu ambayo huwezi kuelewa mwanzoni, lakini baada ya miezi miwili au mitatu, pengine hata mwaka, utayaelewa. Je, hili linawezekanaje? Ni kwa sababu Mungu hawezi kuwafanya watu wawe wakamilifu kwa siku moja au mbili. Wakati mwingi, unaposoma maneno Yake, huenda usielewe papo hapo. Wakati huo, yanaweza kuonekana kama maandishi tu; lazima uyapitie kwa muda kabla ya kuyaelewa. Mungu akiwa Amezungumza mengi sana, unapaswa kufanya kila uwezalo kula na kunywa maneno Yake, kisha, bila ya wewe kutambua, utakuja kuelewa, na bila wewe kutambua, Roho Mtakatifu atakupa nuru. Roho Mtakatifu anapompa mwanadamu nuru, mara nyingi huwa bila ufahamu wa mwanadamu. Yeye hukupa nuru na kukuongoza unapoona kiu na

kutafuta. Kanuni ambayo kwayo Roho Mtakatifu hufanya kazi ina msingi katika maneno ya Mungu ambayo wewe hula na kunywa. Wale wote ambao hawaweki umuhimu katika maneno ya Mungu na daima huwa wenye mtazamo tofauti kwa maneno Yake—wakiamini, katika fikira zao zilizochanganyikiwa, kuwa ni jambo lisilo na athari yoyote wakisoma maneno Yake au la—ni wale ambao hawana uhalisi. Kazi ya Roho Mtakatifu wala utoaji nuru Wake haviwezi kuonekana ndani ya mtu kama huyo. Watu kama hawa wanasairi tu, wanaojifanya na wasio na sifa za kweli, kama Bwana Nanguo wa mfano.^[a]

Bila maneno ya Mungu kama uhalisi wako, huna kimo halisi. Wakati utakapofika wa wewe kujaribiwa, bila shaka utaanguka, na kisha kimo chako cha kweli kitafichuliwa. Lakini wale ambao hutafuta kuingia katika ukweli mara kwa mara, watakapokumbwa na majaribu, watapata kuelewa madhumuni ya kazi ya Mungu. Mtu aliye na dhamiri, na mwenye kiu ya Mungu, anapaswa kuchukua hatua za matendo kumlipa Mungu kwa sababu ya upendo Wake. Wale ambao hawamiliki ukweli hawawezi kusimama imara hata katika mambo madogo. Hiyo ndio tofauti kati ya wale walio na kimo cha kweli na wale wasio na kimo halisi. Je, ni kwa nini kwamba, ingawa wote wanakula na kunywa maneno ya Mungu, wengine wanaweza kusimama imara katika majaribu, huku wengine wanakimbia? Tofauti ya wazi ni kwamba wengine hawana kimo cha kweli; hawana maneno ya Mungu kutumika kama ukweli wao, na maneno Yake hayajakita mizizi ndani yao. Punde tu wanapojaribiwa, wao hufika mwisho wa njia yao. Je, basi ni kwa nini kwamba fulani wanaweza kusimama imara katikati ya majaribu? Ni kwa sababu wanaelewa ukweli na wana maono, na wanaelewa mapenzi ya Mungu na mipango Yake, na hivyo wanaweza kusimama imara katika majaribu. Hiki ni kimo cha kweli, na haya pia ni maisha. Wengine wanaweza pia kusoma maneno ya Mungu, lakini hawayaweki katika vitendo, hawayachukulii kwa uzito; wale ambao hawayachukulii kwa uzito hawaweki umuhimu wowote katika kutenda. Wale ambao hawana maneno ya Mungu kutumika kama ukweli wao hawana kimo cha kweli, na watu kama hao hawawezi kusimama imara katika majaribu.

Maneno ya Mungu yanapotokea, unapaswa kuyapokea mara moja, na kuyala na kuyanywa. Haijalishi wewe unaelewa kiasi gani, mtazamo mmoja ambao lazima ushikilie imara ni kula na kunywa, kujua, na kutebda maneno Yake. Hiki ni kitu ambacho unapaswa kuweza kufanya. Kamwe usijali kuhusu jinsi kimo chako kinavyoweza kuwa kikubwa; lenga tu kula na kunywa maneno Yake. Hiki ndicho mwanadamu anapaswa kushiriki katika. Maisha yako ya kiroho hasa ni kujaribu kuingia katika ukweli wa kula na kunywa maneno ya Mungu na kuyaweka katika vitendo. Sio shughuli yako kulenga juu ya kitu kingine chochote. Viongozi wa kanisa wanapaswa kuwaongoza ndugu zao wote ili wajue jinsi ya kula na kunywa maneno ya Mungu. Hili ndilo jukumu la kila kiongozi wa kanisa. Wawe wachanga au wazee, wote wanapaswa kuzingatia kula na kunywa maneno ya Mungu kama jambo lenye umuhimu mkubwa na

wanapaswa kuwa na maneno Yake mioyoni mwao. Kuingia katika ukweli huu kunamaanisha kuingia katika Enzi ya Ufalme. Leo, watu wengi wanahisi kuwa hawawezi kuishi bila kula na kunywa maneno ya Mungu, na wanahisi kuwa maneno Yake ni mapya bila kujali wakati. Hii inamaanisha kuwa wanaanza kwenda katika njia sahihi. Mungu hutumia maneno kufanya kazi Yake na kumruzuku mwanadamu. Wakati kila mtu anatamani na kuwa na kiu ya maneno ya Mungu, binadamu wataingia katika ulimwengu wa maneno Yake.

Mungu amezungumza mengi sana. Je, ni kiasi gani ambacho wewe umepata kujua? Umeingia kwa kiasi gani? Kama kiongozi wa kanisa hajawaongoza ndugu zake kuingia katika ukweli wa maneno ya Mungu, basi atakuwa hajatimiza wajibu wake, na atakuwa ameshindwa kutekeleza majukumu yake! Ufahamu wako uwe wa kina au wa juu juu, bila kujali kiwango cha ufahamu wako, lazima ujue jinsi ya kula na kunywa maneno Yake, lazima uyazingatie kwa makini sana maneno Yake, na uelewe umuhimu na haja ya kuyala na kuyanywa. Kwa kuwa Mungu amezungumza sana, usipokula na kunywa maneno Yake, au kujaribu kutafuta, au kuyaweka maneno Yake katika vitendo, huku hakuwezi kuitwa kumwamini Mungu. Kwa kuwa unamwamini Mungu, basi lazima uyale na kuyanywa maneno Yake, uyapitie maneno Yake, na uishi kwa kuyadhihirisha maneno Yake. Hii tu ndiyo inayoweza kuitwa imani katika Mungu! Ukisema kwa mdomo wako kwamba unamwamini Mungu lakini huwezi kuyaweka maneno Yake yoyote katika vitendo au kutoa ukweli wowote, huku hakuitwi kumwamini Mungu. Badala yake, ni "kutafuta mkate ili kumaliza njaa." Kuzungumza tu kuhusu ushuhuda mdogo, vitu visivyo na maana, na mambo ya juujuu, bila kuwa hata na ukweli mdogo kabisa: hivi havijumuishi imani katika Mungu, na hujafahamu tu njia sahihi ya kuamini katika Mungu. Kwa nini lazima ule na kunywa maneno mengi ya Mungu iwezekanavyo? Usipokula na kunywa maneno Yake lakini utafute tu kupaa mbinguni, je, huko ni kumwamini Mungu? Je, hatua ya kwanza ambayo mtu amwaminiye Mungu anapaswa kuchukua ni ipi? Ni kwa njia gani ndiyo Mungu humkamilisha mwanadamu? Je, unaweza kukamilishwa bila kula na kunywa maneno ya Mungu? Je, unaweza kuchukuliwa kama mtu wa ufalme bila ya maneno ya Mungu kutumika kama ukweli wako? Je, ni nini hasa maana ya imani katika Mungu? Waumini katika Mungu wanapaswa, angalau, kuwa na tabia njema kwa nje; la muhimu zaidi ni kuwa na maneno ya Mungu. Bila kujali chochote, kamwe huwezi kuyaacha maneno Yake. Kumjua Mungu na kutimiza nia Zake vinafanikishwa kupitia katika maneno Yake. Katika siku zijazo, kila taifa, dhehebu, dini, na sehemu zitashindwa kwa njia ya maneno ya Mungu. Mungu atazungumza moja kwa moja, na watu wote watashikilia maneno ya Mungu mikononi mwao, na kwa njia hii, binadamu watakamilishwa. Ndani na nje, maneno ya Mungu yanapenyeza kote kote: Binadamu watazungumza maneno ya Mungu kwa vinywa vyao, watende kulingana na maneno ya Mungu, na kuweka maneno ya Mungu ndani, wakisalia wamelowa na maneno ya Mungu ndani na nje.

Hivi ndivyo binadamu watakamilishwa. Wale wanaotimiza nia za Mungu na wanaweza kumshuhudia, hawa ni watu wanaomiliki maneno ya Mungu kama ukweli wao.

Kuingia katika enzi ya Neno—Enzi ya Ufalme wa Milenia—ni kazi ambayo inatimizwa leo. Kuanzia sasa kuendelea, fanya mazoezi ya ushirika kuhusu maneno ya Mungu. Ni kwa njia ya kula na kunywa na pia kupitia maneno ya Mungu ndiyo utaweza kuishi kwa kuyadhihirisha maneno ya Mungu. Lazima uwe na uzoefu wa vitendo ili uwashawishi wengine. Ikiwa huwezi kuishi kwa kuadhihirisha ukweli wa maneno ya Mungu, hakuna atakayeshawishika! Wale wote wanaotumiwa na Mungu wanaweza kuishi kwa kuadhihirisha ukweli wa maneno ya Mungu. Ikiwa huwezi kutoa ukweli huu na kumshuhudia Mungu, hii inaonyesha kwamba Roho Mtakatifu hajafanya kazi ndani yako, na kwamba wewe hujakamilishwa. Huu ndio umuhimu wa maneno ya Mungu. Je, wewe una moyo wenye kiu ya maneno ya Mungu? Wale ambao wana kiu ya maneno ya Mungu wana kiu ya ukweli, na watu tu kama hawa tu ndio ambao hubarikiwa na Mungu. Katika siku zijazo, kuna maneno mengi zaidi ambayo Mungu atanena kwa dini zote na madhehebu yote. Kwanza Ananena na kutamka sauti Yake kati yenu ili Awakamilishe kabla ya kusonga mbele kunena na kutamka sauti Yake kati ya watu wa Mataifa ili Awashinde. Kupitia katika maneno Yake, wote watashawishika kwa dhati na kikamilifu. Kupitia katika maneno ya Mungu na ufunuo Wake, tabia potovu ya mwanadamu inapungua, anapata kuonekana kwa mwanadamu, na tabia yake ya uasi inapungua. Maneno hayo hufanya kazi kwa mwanadamu kwa mamlaka na humshinda mwanadamu katika nuru ya Mungu. Kazi ambayo Mungu hufanya katika enzi ya sasa, na vile vile mabadiliko ya kazi Yake, yote yanaweza kupatikana ndani ya maneno Yake. Usiposoma maneno Yake, hutaelewa chochote. Kupitia kula kwako na kunywa maneno Yake, na kupitia kushiriki katika ushirika na ndugu na uzoefu wako halisi, utapata ufahamu kamili wa maneno ya Mungu. Ni hapo tu ndipo utaweza kweli kuishi kwa kudhihirisha ukweli wake.

Tanbihi:

a. Maandishi ya asili hayana maneno “wa mfano.”

Yote Yanafanikishwa Kupitia kwa Neno la Mungu

Mungu huzungumza maneno Yake na kufanya kazi Yake kulingana na enzi tofauti, na katika enzi tofauti, Anazungumza maneno tofauti. Mungu hafuati sheria, ama kurudia kazi ya awali, ama kuhisi hali ya kumbukumbu kwa vitu vilivyopita; ni Mungu ambaye ni mpya kila wakati na hazeera, na kila siku anazungumza maneno mapya. Unapaswa uyafuate yale ambayo lazima yafuatwe leo; haya ni majukumu na kazi ya mwanadamu. Ni muhimu kwamba utendaji uwekwe katika nuru iliyopo na maneno ya Mungu katika siku ya leo. Mungu hafuati masharti, na Anaweza kuzungumza kutoka kwa mitazamo mingi tofauti ili kufanya wazi hekima Yake na

uwezo. Haijalishi ikiwa Anazungumza kutoka kwa mtazamo wa Roho, ama mwanadamu, ama mtu wa tatu—Mungu ni Mungu kila wakati na huwezi kusema kuwa yeye si Mungu kwa sababu ya mtazamo wa mwanadamu ambao Anazungumzia kutoka. Kati ya baadhi ya watu dhana zimetokea kutokana na mitazamo tofauti tofauti ambayo Mungu Anazungumza. Watu hao hawana maarifa ya Mungu, na pia maarifa ya kazi Yake. Iwapo Mungu angezungumza kila wakati kutumia mtazamo mmoja, je mwanadamu hangeweka masharti kuhusu Mungu? Je Mungu Anaweza kukubali mwanadamu kutenda kwa njia hiyo? Haijalishi ni mtazamo gani ambao Mungu Anaongelea, Mungu Ana malengo Yake kwa kila moja. Iwapo Mungu Angeongea kila wakati kwa mtazamo wa Roho, ungeweza kushiriki na Yeye? Hivyo, wakati mwingine Yeye huzungumza kupitia mtu wa tatu ili kukupatia maneno Yake na kukuongoza kwa ukweli. Kila kitu Atendacho Mungu kinafaa. Kwa ufupi, yote yanafanywa na Mungu, na hupaswi kuwa na shaka kuyahusu. Bora tu kwamba Yeye ni Mungu, basi haijalishi kuwa ni mtazamo gani Anaongelea kutoka, Yeye bado ni Mungu. Huu ni ukweli usiobadilika. Njia yoyote Afanyayo kazi, Yeye bado ni Mungu, na dutu Yake haiwezi kubadilika! Petro alimpenda Mungu sana na alikuwa mtu aliyetaka kumridhisha Mungu, lakini Mungu hakumshuhudia kama Bwana ama Kristo, kwani dutu ya kiumbe ni vile ilivyo, na haiwezi badilika. Katika kazi Yake, Mungu hafuati masharti, lakini Anatumia mbinu tofauti kufanya kazi Yake ifanikiwe na kuongeza maarifa ya mwanadamu kumhusu. Kila mbinu Yake ya kazi inamsaidia mwanadamu kumjua, na ni kwa ajili ya kumfanya mwanadamu kamili. Haijalishi ni mbinu gani ya kufanya kazi Yeye hutumia, kila ni ili kumwongeza mwanadamu na kumfanya mtimilifu. Ingawa moja ya mbinu Zake za kazi ilikaa kwa muda mrefu, ni kwa ajili ya kupunguza imani ya mwanadamu Kwake. Hivyo hampaswi kuwa na shaka. Hizi zote ni hatua za kazi ya Mungu, na mnapaswa kuzitii.

Leo, kinachozungumziwa ni kuingia katika hali halisi. Hakuna mazungumzo ya kupaa mbinguni, ama kutawala kama wafalme; yote yazungumziwayo ni harakati za kuingia katika hali halisi. Hakuna njia ya utendaji ya kufuata kuliko hii, na kuongelea kutawala kama wafalme sio tendo la busara. Mwanadamu ana udadisi mkuu, na bado anapima kazi ya Mungu leo kupitia dhana zake za kidini. Baada ya kupitia mbinu nyingi za Mungu za kazi, mwanadamu bado hajui kazi ya Mungu, bado anatafuta ishara na maajabu, na bado anaangalia kama kazi ya Mungu imetimizwa. Je huu sio upofu mkuu? Bila kutimizwa kwa maneno ya Mungu, je bado ungeamini kuwa ni Mungu? Leo, watu wengi kama hao kanisani wanangoja kutazama ishara na maajabu. Wanasema, maneno ya Mungu yakitimizwa, basi yeye ni Mungu; maneno ya Mungu yasipotimizwa, basi yeye si Mungu. Je wewe basi unaamini Mungu kwa sababu ya kutimizwa kwa maneno Yake, ama kwa sababu ni Mungu Mwenyewe? Mtazamo wa mwanadamu wa kumwamini Mungu unafaa kurekebisha! Unapoona kuwa maneno ya Mungu yametimizwa,

unatoroka—je huku ni kuamini katika Mungu? Unapoamini katika Mungu lazima uache kila kitu kwa huruma za Mungu na utii kazi yote ya Mungu. Mungu Alizungumza maneno mengi sana katika Agano la Kale—ni yapi uliyoona kwa macho yako yakitimizwa? Unaweza kusema kuwa Yehova siye Mungu wa kweli kwa sababu hukuona hayo? Hata ingawa huenda maneno mengi yalitimia, mwanadamu hana uwezo wa kuona hilo wazi kwa sababu mwanadamu hana ukweli na haelewi chochote. Wengine hutamani kutoroka wanapohisi kwamba maneno ya Mungu hayajatimia. Jaribu, uone iwapo unaweza kutoroka. Baada ya kutoroka, bado tu utarudi. Mungu anakudhibiti na neno Lake, na ukiacha kanisa na neno la Mungu, hutakuwa na njia ya kuishi. Kama huamini haya, jaribu mwenyewe—unafikiri unaweza tu kuondoka? Roho wa Mungu Anakudhibiti, na huwezi kuondoka. Hii ni amri ya utawala wa Mungu! Kama kuna watu ambao wanataka kujaribu, basi, wanaweza! Unasema huyu mtu si Mungu, basi mtendee dhambi na uone Atakachofanya. Kuna uwezekano kuwa mwili wako hautakufa na bado utakuwa na uwezo wa kula na kuvaa mwenyewe, lakini mawazoni hutaweza kuvumilia; utakuwa na msongo na mateso, hakuna kitu kitakachokuwa uchungu zaidi ya hili. Mwanadamu hawezi kuvumilia kuadhibiwa mawazoni na kuvurugwa—labda unaweza kuvumilia kuumia kwa mwili, lakini huna uwezo wa kuvumilia dhiki ya mawazo na adhabu inayodumu kwa muda mrefu. Leo, watu wengine wanakuwa hasi kwa sababu hawajaweza kuona ishara na maajabu yoyote, ilhali hakuna anayethubutu kukimbia bila kujali jinsi anavyokuwa hasi, kwani Mungu humdhibiti mwanadamu kwa neno Lake. Licha ya kutokuweco ujio wa ukweli, ilhali hakuna anayeweza kutoroka. Je haya si matendo ya Mungu? Leo, Mungu amekuja duniani kumpa mwanadamu maisha. Yeye hawezi kukubembeleza, vile watu wanavyofikiria kwa kukuonyesha ishara na maajabu ili kuhakikisha uhusiano wa amani kati ya Mungu na mwanadamu. Wale wote ambao lengo lao halielekei maisha, na badala yake wanakuwa makini kumfanya Mungu aonyeshe ishara na maajabu, ni Mafarisayo! Wakati huo, ni Mafarisayo ndio waliompiga Yesu misumari msalabani; ukimpima Mungu kulingana na mtazamo wa imani yako kwa Mungu, kumwamini Mungu maneno Yake yanapotimizwa, na kuwa na shaka na hata kumkufuru Mungu yasipotimizika, je basi huko si kumpiga misumari msalabani? Watu kama hao ni wazembe katika kazi zao, na wanasherekea kilafi kwa raha!

Kwa upande mmoja, shida kubwa na mwanadamu ni kwamba haijui kazi ya Mungu. Ingawa tabia ya mwanadamu sio ile ya kukataa, ni ile ya shaka; hakatai, lakini pia hawezi kukiri kikamilifu. Watu wakiwa na maarifa kamilifu ya kazi ya Mungu, basi hawatatoroka. Kwa upande mwingine, ni kwamba mwanadamu hajui hali halisi. Leo, ni kwa neno la Mungu, ndio kila mmoja ameshiriki; hakika, baadaye usingoje kuona ishara na maajabu. Nawaambia waziwazi: Katika hatua ya sasa, kile una uwezo wa kuona ni maneno ya Mungu, na ingawa hakuna jambo la hakika, maisha ya Mungu bado inaweza kuundwa ndani ya mwanadamu. Ni

kazi hii ndiyo kazi kuu ya Ufalme wa Milenia, na iwapo huwezi kuiona kazi hii, basi utakuwa mnyonge na kuanguka chini, utateremka kukiwa na majaribu na zaidi ya haya, utachukuliwa kama mfungwa na Shetani. Mungu Amekuja ulimwenguni hasa kuzungumza maneno Yake; unachoshiriki nacho ni neno la Mungu, uonacho ni neno la Mungu, usikiacho ni neno la Mungu, unachokaa nacho ni neno la Mungu, unachopitia ni neno la Mungu, na Mungu aliyepata mwili huyu kimsingi hutumia neno kumfanya mwanadamu kamili. Yeye haonyeshi ishara na maajabu, na hasa hafanyi kazi ambayo Yesu Alifanya hapo awali. Ingawa wao ni Mungu, na wote ni mwili, huduma Zao sio sawa. Yesu Alipokuja, Alifanya pia baadhi ya sehemu ya kazi ya Mungu, na kuongea baadhi ya maneno—lakini ni kazi gani kuu Aliyokamilisha? Alichokamilisha hasa ni kazi ya kusulubishwa. Akawa mfano wa mwili wenye dhambi ili kukamilisha kazi ya kusulubiwa na kuwakomboa wanadamu wote, na ilikuwa kwa ajili ya dhambi zote za binadamu, ndio Alitumika kama sadaka ya dhambi. Hii ndiyo kazi hasa Aliyokamilisha. Hatimaye, Alileta njia ya msalaba ili kuwaongoza wale waliokuja baadaye. Yesu Alipokuja, ilikuwa kimsingi kukamilisha kazi ya ukombozi. Aliwakomboa binadamu wote, na kuleta injili ya ufalme wa mbinguni kwa mwanadamu, na zaidi, Alileta njia ya ufalme wa mbinguni. Kwa sababu hii, waliokuja baada ya yote walisema, “Tunapaswa tutembe njia ya msalaba, na tujitoe kama kafara kwa ajili ya msalaba.” Bila shaka, hapo mwanzo Yesu pia Alifanya kazi nyingine na kuongea baadhi ya maneno ili kumfanya mwanadamu atubu na kukiri dhambi zake. Lakini huduma Yake ilikuwa bado ni kusulubiwa, na miaka mitatu na nusu Aliyotumia kuhubiri njia ilikuwa katika matayarisho ya kusulubiwa kulikokuja baadaye. Mara kadhaa ambazo Yesu Alisali zilikuwa pia ni kwa ajili ya kusulubishwa. Maisha ya mwanadamu wa kawaida Aliyoishi na miaka thelathini na tatu na nusu aliyoishi duniani yalikuwa kimsingi kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kusulubishwa, yalikuwa ya kumpa nguvu ya kutekeleza kazi hii, na kwa sababu hii Mungu Alimwaminia kazi ya kusulubiwa. Leo ni kazi gani ambayo Mungu katika mwili atakamilisha? Leo Mungu Amekuwa mwili kimsingi ili kukamilisha kazi ya “Neno kuonekana katika mwili,” kutumia neno kumfanya mwanadamu kamili, na kumfanya mwanadamu kukubali ushughulikiaji wa neno na usafishaji wa neno. Katika maneno Yake, anakufanya kupata kupewa na kupata uzima; katika maneno Yake, unaona kazi Yake na matendo. Mungu Anatomia neno kukuadibu na kukutakasa, na hivyo ukipata ugumu wa maisha, ni pia kwa sababu ya neno la Mungu. Leo, Mungu hafanyi kazi kwa kutumia mambo ya hakika, ila ni kwa maneno. Baada tu ya neno Lake kuja juu yako ndipo Roho Mtakatifu Atafanya kazi ndani yako na kukufanya upate uchungu ama uhisi utamu. Ni neno la Mungu pekee ndilo linaloweza kukuleta katika hali halisi, na ni neno la Mungu pekee ndilo linaloweza kukufanya mkamilifu. Kwa hivyo, angalau lazima uelewe hili: Kazi inayofanywa na Mungu katika siku za mwisho kimsingi ni kutumia neno Lake kumfanya kila mwanadamu kamili na kumwongoza mwanadamu. Kazi yote Anayofanya ni kupitia kwa neno; Hatumii ukweli kuadibu. Kuna wakati ambapo watu wengine humpinga

Mungu. Mungu hasababishi ukosefu mkubwa wa starehe kwako, mwili wako hauadibiwi wala wewe kupitia ugumu—lakini pindi tu neno Lake linapokuja juu yako, na kukutakasa, hutaweza kuvumilia. Je si hivyo ndivyo ilivyo? Wakati wa “watendaji huduma” Mungu Alisema mwanadamu atupwe katika shimo lisilo na mwisho. Mwanadamu aliweza kufika kwenye shimo lisilo na mwisho? Kupitia kwa maneno tu kumtakasa mwanadamu, mwanadamu aliingia kwenye shimo lisilo na mwisho. Kwa hivyo, katika siku za mwisho, Mungu anapokuwa mwili, kimsingi Anatumia neno kukamilisha yote na kufanya yote yawe wazi. Katika maneno Yake pekee ndipo unaweza kuona kile Alichio; ni katika maneno Yake pekee ndiyo unaweza kuona kwamba yeye ni Mungu Mwenyewe. Mungu katika mwili Anapokuja duniani, hafanyi kazi nyingine ila kuongea maneno—hivyo basi hakuna haja ya kutumia uhakika; maneno yanatosha. Hii ni kwa sababu Amekuja kimsingi kufanya kazi hii, kumruhusu mwanadamu aone nguvu Zake na ukuu ulio kwenye neno Lake, kumruhusu mwanadamu kuona kupitia kwa maneno Yake jinsi Alivyojificha kwa unyenyekevu, na kumruhusu mwanadamu kujua ukamilifu Wake kupitia kwa maneno Yake. Kila kitu Alichio nacho na kile Alichio kiko katika maneno Yake, hekima Yake na ajabu yako katika maneno Yake. Katika hii ndipo unapofanywa kuona mbinu nyingi ambazo Mungu anatumia kuongea maneno Yake. Kazi ya Mungu nyingi katika wakati huu wote imekuwa kutoa, ufunuo, na kushughulika mwanadamu. Hatoi laana kwa mwanadamu kijuu juu, na hata Akifanya hivyo, ni kupitia kwa neno. Na hivyo, katika enzi hii ya Mungu kuwa mwili, usijaribu kuona Mungu akiponya wagonjwa na kufukuza mapepo tena, usijaribu kila mara kuona ishara—hakuna haja! Ishara hizo haziwezi kumfanya mwanadamu kamili! Kuongea wazi: Leo Mungu wa kweli Mwenyewe wa mwili Anaongea tu, na hatendi. Huu ni ukweli! Anatumia maneno kukufanya mkamilifu, na Anatumia maneno kukulisha na kukunyunyizia. Pia Anatumia maneno kufanya kazi, na Anatumia maneno badala ya uhakika kukufanya ujue ukweli Wake. Kama una uwezo wa kutazama aina hii ya kazi ya Mungu, basi itakuwa vigumu kuwa wa kutoonyesha hisia. Badala ya kulenga vitu vilivyo vibaya, mnapaswa tu kulenga yale yaliyo mazuri—hivyo ni kusema, bila kujali kama maneno ya Mungu yamekamilika au la, ama iwapo kuna majilio ya ukweli ama haupo, Mungu anamfanya mwanadamu kupata uzima kutoka kwa maneno Yake, na hii ndiyo ishara kuu kushinda zote, na hata zaidi, ni ukweli usiopingika. Huu ndio ushahidi bora wa kupata ufahamu kumhusu Mungu, na ni ishara hata kuu kushinda ishara. Maneno haya pekee yanaweza kumfanya mwanadamu kamili.

Pindi tu Enzi ya Ufalme ilipoanza, Mungu alianza kuachilia Maneno Yote. Katika siku za baadaye, maneno haya yataendelea kutimizwa, na katika wakati huo, mwanadamu atakua katika uzima. Matumizi ya neno na Mungu kufichua tabia potovu ya mwanadamu ni ya kweli zaidi, na ni ya lazima zaidi, na Hatumii chochote ila neno kufanya kazi Yake ili kuifanya imani ya mwanadamu iwe kamili, kwani leo ni Enzi ya Neno, na inahitaji imani, uamuzi na ushirikiano

wa mwanadamu. Kazi ya Mungu katika mwili wa siku za mwisho ni kutumia neno Lake kutumikia na kukimu mahitaji ya mwanadamu. Ni baada tu ya Mungu katika mwili kumaliza kuongea maneno Yake ndipo yatakapoanza kutimika. Wakati Anapooongea, maneno Yake hayatimiliki, kwani Anapokuwa katika hatua ya mwili, maneno Yake hayawezi kutimika, na hii ni ili mwanadamu aweze kuona kuwa Mungu ni mwili na sio Roho, ili mwanadamu aweze kutazama hali halisi ya Mungu kwa macho yake Mwenyewe. Katika ile siku ambayo kazi Yake imekamilika, wakati ambao maneno yote yanayopaswa kunenwa na Yeye duniani yamenenwa, maneno Yake yataanza kutimika. Sasa sio enzi ya utimizaji wa maneno ya Mungu, kwa kuwa Hajamaliza kuongea maneno Yake. Kwa hivyo ukiona kuwa Mungu bado Ananena maneno yake duniani, usingoje kutimizwa kwa maneno Yake; Mungu Anapokoma kunena maneno Yake, na wakati kazi Yake duniani imekamilika, huo ndio utakuwa wakati ambao maneno Yake yanaanza kutimika. Katika maneno Anayozungumza duniani, kunayo, katika mtazamo mmoja, utoaji wa uzima, na katika mtazamo mwingine, kuna unabii—unabii wa vitu vitakavyokuja, wa vitu vitakavyofanywa, na vya vitu ambavyo bado havijatimizwa. Kulikuwa pia na unabii katika maneno ya Yesu. Katika mtazamo mmoja, Alitoa uzima, na katika mtazamo mwingine Alinena unabii. Leo, hakuna mazungumzo ya kutekeleza maneno na uhakika kwa wakati mmoja, kwani tofauti kati ya yale yanayoweza kuonekana na macho ya mwanadamu na yale yanayotendwa na Mungu ni kubwa mno. Inaweza kusemwa tu kwamba, mara kazi ya Mungu inapokamilika, maneno Yake yatatimika, na mambo ya hakika yatakuja baada ya maneno. Duniani, Mungu katika mwili wa siku za mwisho anafanya huduma ya neno, na kwa kufanya huduma ya neno, Anazungumza maneno pekee, na hajali kuhusu mambo mengine. Mara kazi ya Mungu itakapobadilika, maneno Yake yataanza kutimika. Leo, maneno yanatumiwa kwanza kukufanya mkamilifu; Atakapopokea utukufu katika ulimwengu mzima, utakuwa wakati ambao kazi Yake imekamilika, wakati maneno yote ambayo yanapaswa kuzungumzwa yatakuwa yamezungumzwa, na maneno yote yamekuwa ukweli. Mungu amekuja duniani wakati wa siku za mwisho ili kutekeleza huduma ya neno ili mwanadamu amtambue, na ili mwanadamu aone kile Alicheo, na aone hekima Yake na matendo Yake yote ya maajabu kutoka kwa neno Lake. Katika Enzi ya Ufalme, Mungu anatumia neno kimsingi kushinda watu wote. Baadaye neno Lake litakuja katika kila dini, kikundi, taifa na madhehebu; Mungu hutumia neno kushinda, kuwafanya wanadamu wote waone kuwa neno Lake lina mamlaka na nguvu—na kwa hivyo leo, mnakumbana tu neno la Mungu.

Maneno ambayo Mungu Alizungumza katika enzi hii ni tofauti na yale yaliyozungumzwa katika Enzi ya Sheria, na kwa hivyo, pia yako tofauti na maneno yaliyonenwa katika Enzi ya Neema. Katika Enzi ya Neema, Mungu hakufanya kazi ya neno, lakini Alieleza tu usulubisho ili kuwakomboa binadamu wote. Biblia inaelezea tu ni kwa nini Yesu alikuwa Asulubiwe, na

mateso ambayo Alipitia kwenye msalaba, na jinsi mwanadamu anapaswa kusulubiwa kwa ajili ya Mungu. Katika enzi hiyo, kazi yote iliyofanywa na Mungu ilikuwa kuhusu usulubisho. Katika Enzi ya Ufalme, Mungu katika mwili Anazungumza maneno ili kushinda wale wote wanaomwamini. Huu ni, “Neno kuonekana katika mwili”; Mungu amekuja katika siku za mwisho ili kufanya kazi hii, ambayo ni kusema, Amekuja kutimiza umuhimu wenyewe wa Neno kuonekana katika mwili. Ananena tu maneno, na majilio ya ukweli ni chache. Hii ndiyo dutu kamili ya Neno kuonekana katika mwili, na wakati Mungu katika mwili Anaponena maneno Yake, huku ndiko kuonekana kwa Neno katika Mwili, na ni Neno kuja katika mwili. “Mwanzoni kulikuwa na Neno, na Neno alikuwa na Mungu, na Neno alikuwa Mungu, na Neno likawa mwili.” Hii (kazi ya kuonekana kwa Neno katika mwili) ni kazi ambayo Mungu atatimiza katika siku za mwisho, na ni sura ya mwisho ya mpango Wake mzima wa uongozi, kwa hivyo Mungu lazima Aje duniani na kudhihirisha maneno Yake katika mwili. Yale yanayofanywa leo, yale yatakayofanywa baadaye, yale yatakayotimizwa na Mungu, hatima ya mwisho mwanadamu, wale wataaokolewa, wale watakaangamizwa, na mengine mengi—kazi hii ambayo lazima itimizwe mwishowe imesemwa wazi, na yote ni kwa ajili ya kutimiza umuhimu halisi wa Neno kuonekana kwa mwili. Amri za utawala na katiba ambayo ilipeanwa hapo awali, wale ambao wataangamizwa, wale watakaolingia katika mapumziko—maneno haya lazima yatimizwe. Hii ni kazi iliyotimizwa kimsingi na Mungu katika mwili katika siku za mwisho. Anawafanya watu waelewe kule ambako wale waliopangiwa na Mungu wanapaswa kuwa na wale wasiopangiwa na Mungu wanapaswa kuwa, jinsi ambavyo watu Wake na wana Wake watawekwa kwenye vikundi, ni nini kitaifanyikia Uyahudi, ni nini kitaufanyikia Misri—katika siku za usoni, kila mojawapo ya maneno haya yatatimizwa. Hatua za kazi za Mungu zinaharakishwa. Mungu hutumia neno kama mbinu ya kumfichulia mwanadamu kinachopaswa kufanyika katika kila enzi, kinachopaswa kufanywa na Mungu katika mwili wa siku za mwisho, na huduma Yake ambayo inapaswa kufanywa, na maneno haya ni kwa ajili ya kutimiza umuhimu hasa wa Neno kuonekana kwa mwili.

Nimesema hapo awali kuwa “Wale wote wanaoangazia kuona ishara na maajabu watatelekezwa; wao sio wale watakaofanywa wakamilifu.” Nimenena maneno mengi sana, ilhali mwanadamu hana maarifa hata kidogo ya kazi hii, na, baada ya kufika katika hatua hii, bado mwanadamu anaulizia ishara na maajabu. Je, kuamini kwako kwa Mungu ni harakati ya kuona ishara na maajabu, au ni kwa sababu ya kupata uzima? Yesu pia Alinena maneno mengi, na mengine bado hayajatimika leo. Je unaweza kusema kuwa Yesu sio Mungu? Mungu alishuhudia kuwa Yeye ni Kristo na ni Mwana mpendwa wa Mungu. Je unaweza kukataa haya? Leo, Mungu anazungumza tu maneno, na iwapo huna uwezo wa kufahamu kabisa, basi huwezi kusimama kidete. Je unamwamini kwa sababu Yeye ni Mungu, au unamwamini kwa msingi kwamba

maneno Yake yatatimika au la? Je unaamini katika ishara na maajabu, au unaamini katika Mungu? Leo, Haonyeshi ishara na maajabu—je Yeye kweli ni Mungu? Iwapo maneno Anayonena hayatimiki, je Yeye kweli ni Mungu? Je dutu ya Mungu inaamuliwa na iwapo maneno Anenayo yatatimika au hapana? Ni kwa nini watu wengine daima hungoja kutimika kwa maneno ya Mungu kabla ya kumwamini? Je hii si maana kwamba hawamjui? Wote walio na dhana za aina hii ni watu wanaomkana Mungu. Wanatumia dhana kumpima Mungu; maneno ya Mungu yakitimika wanamwamini Mungu, na yasipotimika hawamwamini Mungu; na kila wakati wanatafuta kuona ishara na maajabu. Je wao si Mafarisayo wa wakati wa sasa? Kama unaweza ama huwezi kusimama imara kunategemea iwapo unamjua ama humjui Mungu wa kweli—hili ni muhimu! Jinsi ulivyo ukuu wa uhalisi wa neno la Mungu ndani Yako, ndivyo ulivyo ukubwa wa maarifa yako kuhusu uhakika wa Mungu, na ndivyo utaweza kusimama kidete katika majaribu. Kadri unavyotazamia kuona ishara na maajabu, ndivyo utakavyokosa zaidi kusimama imara, na utaanguka katika majaribu. Ishara na maajabu sio msingi; uhakika wa Mungu tu ndio uzima. Watu wengine hawajui matokeo yanayotokana na kazi ya Mungu. Wanaishi katika mshangao kila siku, wakikosa kutafuta ufahamu wakazi ya Mungu. Harakati zao ni kumfanya Mungu atimize mapenzi yao, na ni baada tu ya haya ndio wawe makini katika imani yao. Wanasema kuwa watautafuta uzima iwapo maneno ya Mungu yatatimika, lakini iwapo maneno ya Mungu hayatatimika, basi hakuna uwezekano wa wao kuutafuta uzima. Mwanadamu anafikiri kuwa imani kwa Mungu ni kutafuta kuona ishara na maajabu na harakati ya kupanda mbinguni na mbingu ya tatu. Hakuna asemaye kuwa imani yake kwa Mungu ni harakati ya kuingia katika ukweli, kutafuta uzima, na kutafuta kupatwa na Mungu. Harakati ya aina hii ina thamani gani? Wale wasiofuata ufahamu wa Mungu na kuridhika kwa Mungu ni watu ambao hawamwamini Mungu, ni watu ambao hukufuru Mungu!

Je sasa mnaelewa imani kwa Mungu ni nini? Je kuamini Mungu ni kuona ishara na maajabu? Je ni kupanda mbinguni? Kuamini Mungu sio rahisi hata kidogo. Zile desturi za kidini lazima zitakaswe; kufuata uponyaji wa wagonjwa na kukemea mapepo, kuisitiza ishara na maajabu, kutamani zaidi neema, amani na furaha ya Mungu, kufuata mandhari na raha za mwili—haya ni matendo ya kidini, na matendo haya ya aina hii ya kidini ni aina ya imani isiyo dhahiri. Leo, imani ya kweli kwa Mungu ni nini? Ni kukubali neno la Mungu kama ukweli wa maisha yako na kumjua Mungu kutoka kwa neno Lake ili uufikie upendo wa kweli Kwake. Kuondoa tashwishi: Imani katika Mungu ni ili uweze kumtii Mungu, kumpenda Mungu, na kufanya majukumu ambayo kiumbe wa Mungu anapaswa kufanya. Hili ndilo lengo la kuamini katika Mungu. Lazima upate ufahamu wa upendo wa Mungu, jinsi Mungu anavyostahili heshima, jinsi, katika viumbe Vyake, Mungu anafanya kazi ya wokovu na kuwafanya wakamilifu—haya ndiyo mahitaji ya chini kabisa ya imani yako katika Mungu. Imani katika

Mungu hasa ni mabadiliko kutoka kwa maisha ya mwili kwenda kwa maisha ya kumpenda Mungu; kutoka katika kuishi ndani ya upotovu hadi katika kuishi ndani ya maisha ya maneno ya Mungu; ni kutoka kumilikiwa na Shetani na kuishi chini ya utunzaji na ulinzi wa Mungu, ni kuweza kupata kumtii Mungu na sio kuutii mwili, ni kukubali Mungu kuupata moyo wako wote, kukubali Mungu akufanye mkamilifu, na kujitoa kutoka kwa tabia potovu ya kishetani. Imani kwa Mungu kimsingi ni kwa kuwezesha nguvu na sifa za Mungu kudhihirishwa kwako, ili uweze kufanya mapenzi ya Mungu, na kutimiza mpango wa Mungu, na uweze kutoa ushuhuda kwa Mungu mbele ya Shetani. Imani kwa Mungu haipaswi kuwa kwa ajili ya kuona ishara na maajabu, wala haipaswi kuwa kwa ajili ya mwili wako mwenyewe. Inapaswa kuwa kwa ajili ya kutafuta kumjua Mungu, na kuweza kumtii Mungu, na kama Petro, kumtii mpaka kifo. Hili ndilo imani hiyo inapaswa kupata. Kula na kunywa neno la Mungu ni kwa ajili ya kumjua Mungu na kumtosheleza Mungu. Kula na kunywa neno la Mungu kunakupa maarifa kubwa ya Mungu, na ndipo tu utakapoweza kumtii. Ukiwa na maarifa ya Mungu tu ndipo unapoweza kumpenda, na hili ndilo lengo ambalo mwanadamu anapaswa kuwa nalo katika imani yake kwa Mungu. Iwapo katika imani yako kwa Mungu, unajaribu kila wakati kuona ishara na maajabu, basi mtazamo wa imani hii kwa Mungu si sahihi. Imani kwa Mungu ni hasa kukubali neno la Mungu kama ukweli wa maisha. Ni kuweka tu katika matendo maneno ya Mungu kutoka kwa kinywa Chake na kuyatekeleza mwenyewe ndiko kupatikana kwa lengo la Mungu. Katika kuamini Mungu, mwanadamu anapaswa kutafuta kufanywa mkamilifu na Mungu, kuweza kujiwasilisha kwa Mungu, na kumtii Mungu kikamilifu. Iwapo unaweza kumtii Mungu bila kulalamika, kuyajali mapenzi ya Mungu, kupata kimo cha Petro, na kuwa na mtindo wa Petro ilivyozungumziwa na Mungu, basi hapo ndipo utakuwa umefanikiwa katika imani kwa Mungu, na itadhihirisha kuwa umepatwa na Mungu.

Mungu anafanya kazi Yake katika ulimwengu mzima. Wote wanaoamini katika Yeye lazima walikubali neno Lake, na kula na kunywa neno Lake; hakuna atakayepatwa na Mungu kwa kuona ishara na maajabu yanayoonyeshwa na Mungu. Katika enzi zote, Mungu ametumia neno kila wakati kumfanya mwanadamu mkamilifu. Hivyo hampaswi kuweka mawazo yenu yote kwa ishara na maajabu, ila unapaswa kutafuta kufanywa mkamilifu na Mungu. Katika Enzi ya Sheria ya Agano la Kale, Mungu alinena baadhi ya maneno, na katika Enzi ya Neema, Yesu pia Alinena maneno mengi. Baada ya Yesu kunena maneno haya mengi, mitume na wanafunzi wa baadaye waliwaongoza watu kutenda kulingana na amri zilizotolewa na Yesu na wakapata uzoefu kulingana na maneno na kanuni zilizozungumziwa na Yesu. Katika siku za mwisho, Mungu hasa hutumia neno kumfanya mwanadamu kuwa mkamilifu. Hatumii ishara na maajabu kumdhulumu mwanadamu, ama kumshawishi mwanadamu; hii haiweki wazi nguvu za Mungu. Iwapo Mungu angeonyesha tu ishara na maajabu, basi hakungekuwa na uwezo wa kuweka wazi

ukweli wa Mungu, na hivyo haingewezekana kumfanya mwanadamu mkamilifu. Mungu hamfanyi mwanadamu mkamilifu kwa kutumia ishara na maajabu, ila Anatumia neno kunyunyizia na kumchungu mwanadamu, na baada ya haya kunapatikana utiifu kamili wa mwanadamu na ufahamu wa mwanadamu kuhusu Mungu. Hili ndilo lengo la kazi Anayofanya na maneno Anenayo. Mungu hatumii mbinu ya kuonyesha ishara na maajabu ili kumfanya mwanadamu kamili—Anatumia maneno, na Anatumia mbinu nyingi za kazi kumfanya mwanadamu kamili. Iwe ni usafishaji, kushughulikia, upogoaji, ama kupewa maneno, Mungu hunena kutoka taswira nyingi tofauti kumfanya mwanadamu kamili, na kumpa mwanadamu maarifa kuu ya kazi, hekima na ajabu ya Mungu. Mwanadamu anapofanywa mkamilifu katika wakati ambao Mungu Anamaliza enzi katika siku za mwisho, basi atakuwa amehitimu kuona ishara na maajabu. Unapokuja kumjua Mungu na uweze kumtii Mungu bila kujali Anachofanya, hutakuwa tena na mawazo kumhusu Yeye unapooni ishara na maajabu. Kwa sasa, wewe ni mpotovu na huwezi kuwa na utiifu kamili kwa Mungu—je umehitimu kuona ishara na maajabu? Wakati ambao Mungu anaonyesha ishara na maajabu ndio wakati ambao Mungu anamwadhibu mwanadamu, na pia wakati ambao enzi inabadilika, na zaidi, wakati ambapo enzi inatamatika. Wakati ambao kazi ya Mungu inatekelezwa kama kawaida, Haonyeshi ishara na maajabu. Kuonyesha ishara na maajabu ni jambo rahisi mno, lakini hiyo si kanuni ya kazi ya Mungu, wala si lengo la usimamizi wa Mungu wa mwanadamu. Iwapo mwanadamu angeona ishara na maajabu, na kama mwili wa kiroho wa Mungu ungemtokea mwanadamu, je watu wote hawangeweza “kuamini” katika Mungu? Nimesema hapo awali kuwa kikundi cha washindi wanapatwa kutoka Mashariki, washindi ambao wanatoka katika mashaka makubwa. Je maneno haya yana maana gani? Yanamaanisha kuwa watu hao ambao wamepatwa waliamini kwa kweli tu baada ya kupitia hukumu na kuadibu, na kushughulikiwa na kupogolewa, na aina yote ya usafishaji. Imani ya watu kama hao si isiyo dhahiri na dhahania, bali ni ya kweli. Hawajaona ishara na maajabu yoyote, ama miujiza yoyote; hawazungumzi kuhusu barua ngumu kueleweka na kanuni, ama mitazamo ya muhimu sana; badala yake, wana ukweli, na maneno ya Mungu, na maarifa ya kweli kuhusu ukweli wa Mungu. Je kikundi hiki hakina uwezo wa kuweka wazi nguvu za Mungu? Kazi ya Mungu katika siku za mwisho ni ya uhakika. Katika enzi ya Yesu, hakuja kumfanya mwanadamu awe kamili, ila kumkomboa mwanadamu, na hivyo Alionyesha miujiza kadhaa ili kufanya watu wamfuate. Kwani Yeye hasa Alikuwa kukamilisha kazi ya kusulubiwa, na kuonyesha ishara haikuwa sehemu ya huduma Yake. Ishara na maajabu hayo yalikuwa ni kazi ambayo yalifanyika ili kufanya kazi Yake iwe na matokeo ya kufaa; hayo yalikuwa tu kazi ya ziada, na hayakuwakilisha kazi ya enzi nzima. Katika Enzi ya Sheria ya Agano la Kale, Mungu pia Alionyesha ishara na maajabu kadhaa—lakini kazi Anayofanya Mungu leo ni kazi halisi, na kwa uhakika hawezi kuonyesha ishara na maajabu sasa. Kama Angeonyesha ishara na maajabu, kazi Yake halisi ingevurugwa, na hangeweza kufanya kazi

nyingine zaidi. Iwapo Mungu angesema neno litumiwe kumfanya mwanadamu kuwa kamili, lakini pia Aonyeshe ishara na maajabu, basi mwanadamu kumwamini ama kutomwamini kweli kungeweza kuwekwa wazi? Hivyo, Mungu hafanyi vitu vya aina hiyo. Kuna udini mwingi sana katika mwanadamu; Mungu amekuja katika nyakati za mwisho ili kutoa dhana zote za kidini na vitu visivyo vya kidunia ndani ya mwanadamu, na kumfanya mwanadamu ajue ukweli wa Mungu. Amekuja kutoa picha ya Mungu ambayo ni ya dhahania na bunifu—picha ya Mungu ambaye, kwa maneno mengine, hayupo hata kidogo. Na hivyo, sasa kitu cha pekee kilicho cha thamani ni wewe kuwa na ufahamu kuhusu hali halisi! Ukweli unashinda kila kitu. Unamiliki ukweli kiasi gani leo? Je, kila kitu kinachoonyesha ishara na maajabu ni Mungu? Roho wabaya pia wanaweza kuonyesha ishara na maajabu; je, hawa wote ni Mungu? Katika imani yake kwa Mungu, kile anachotafuta mwanadamu ni ukweli, anachotafuta ni uzima, na sio ishara na maajabu. Hivi ndivyo linavyopaswa kuwa lengo la wote wanaoamini katika Mungu.

Wale Wanaompenda Mungu Kwa Kweli Ni Wale Wanaoweza Kutii Utendaji Wake Kabisa

Kuwa na ujuzi wa utendaji na kuwa na uwezo wa kuona wazi kazi ya Mungu—yote haya yanaonekana katika maneno Yake. Ni katika maneno ya Mungu tu ndio unaweza kupata nuru, hivyo unapaswa kujitayarisha na maneno Yake zaidi. Gawa ufahamu wako kutoka kwa maneno ya Mungu katika ushirika, na kupitia katika ushirika wako wengine wanaweza kupata nuru na unaweza kuwaongoza watu kwenye njia—njia hii ni ya utendaji. Kabla ya Mungu kuanzisha mazingira kwa ajili yenu, kila mmoja wenu lazima kwanza ajitayarishe na maneno Yake. Hiki ni kitu ambacho kila mtu anapaswa kufanya—ni kipaumbele cha haraka. Kitu cha kwanza cha kufanya ni kuwa na uwezo wa kula na kunywa maneno Yake. Kwa mambo ambayo huwezi kufanya, tafuta njia ya kutenda kutoka kwa maneno Yake, na angalia katika maneno Yake masuala yoyote ambayo hujui au matatizo yoyote uliyo nayo. Yafanye maneno ya Mungu yawe ruzuku yako, na uyaruhusu yaweze kukusaidia katika kutatua shida na matatizo yako ya vitendo; pia yaruhusu maneno Yake yawe msaada wako katika maisha. Mambo haya yanahitaji jitihada kwa upande wako. Katika kula na kunywa neno la Mungu, lazima ufanikishe matokeo; lazima uweze kuutuliza moyo wako mbele Yake, na kutenda kulingana na maneno Yake unapokabili masuala. Wakati hujakutana na masuala yoyote, kula na kunywa tu. Wakati mwingine unaweza kuomba na kutafakari juu ya upendo wa Mungu, kuwa na ushirika juu ya ufahamu wako wa maneno Yake, na kuwasiliana juu ya kupata nuru na kupata mwanga unaoupitia ndani yako mwenyewe na majibu ambayo umekuwa nayo unapoyasoma matamko haya. Aidha, unaweza kuwapa watu suluhisho. Hili pekee ndilo la utendaji. Lengo la kufanya hili ni kuyaruhusu maneno ya Mungu kuwa utoaji wako wa vitendo.

Kitika kipindi cha siku moja, unatumia saa ngapi kwa hakika mbele ya Mungu? Ni kiasi gani cha siku yako kinachotolewa kwa Mungu? Ni kiasi gani kinachopewa kwa mwili? Moyo wa mtu kuelekea daima kwa Mungu ndiyo hatua ya kwanza kwenye njia sahihi ya kufanywa mkamilifu na Mungu. Unaweza kuutoa moyo wako na mwili na upendo wako wote wa kweli kwa Mungu, uyaweke mbele Zake, kuwa mtiifu kabisa Kwake, na kufikiria kabisa mapenzi Yake. Si kwa ajili ya mwili, si kwa ajili ya familia, wala si kwa ajili ya matamania yako mwenyewe, bali ni kwa ajili ya maslahi ya nyumba ya Mungu. Katika kila kitu unaweza kuchukua neno la Mungu kama kanuni, kama msingi. Hivyo, malengo yako na mtazamo wako yote yatakuwa mahali sahihi, na utakuwa mtu ambaye anapata sifa za Mungu mbele Zake. Wale ambao Mungu hupenda ni watu ambao ni kamili kabisa, watu ambao wamejitolea kwake na hakuna mwingine. Wale ambao Yeye huwachukia ni watu ambao wako shingo upande kumhusu, na ambao wanaasi dhidi Yake. Anawachukia wale wanaomwamini na daima wanataka kumfurahia, lakini hawawezi kujitumia kabisa kwa ajili Yake. Anawachukia wale wanaosema wanampenda lakini wanaomuasi mioyoni mwao. Anawachukia wale wanaotumia maneno matamu ili wafanye udanganyifu. Wale ambao hawajitolei kwa kweli kwa Mungu au hawana utiifu wa kweli Kwake ni watu wasio waaminifu; wao kwa kawaida ni wenye kiburi sana. Wale ambao hawawezi kuwa watiifu kwa kweli mbele ya Mungu wa kawaida, wa vitendo hata ni wenye kiburi zaidi, na hasa wao ni uzao mtiifu wa malaika mkuu. Wale ambao kwa kweli hujitumia wenyewe kwa ajili ya Mungu huweka nafsi zao zote mbele Yake. Wao hutii kwa kweli matamshi Yake yote, na wana uwezo wa kuweka maneno Yake katika matendo. Wao hufanya maneno ya Mungu kuwa msingi wa kuwepo kwao, na wanaweza kutafuta kwa kweli sehemu za matendo katika neno la Mungu. Huyu ni mtu ambaye kwa kweli anaishi mbele ya Mungu. Ikiwa unachofanya ni cha manufaa kwa maisha yako, na kwa njia ya kula na kunywa maneno Yake, unaweza kukidhi mahitaji yako ya ndani na upungufu ili tabia yako ya maisha inabadilishwa, basi hii itatimiza mapenzi ya Mungu. Ikiwa unatenda kulingana na mahitaji ya Mungu, ikiwa huuridhishi mwili lakini unaridhisha mapenzi Yake, huku ni kuingia katika uhalisi wa maneno Yake. Wakati unazungumza juu ya kuingia katika uhalisi wa maneno ya Mungu kwa kweli zaidi, kunamaanisha unaweza kutekeleza wajibu wako na kukidhi mahitaji ya Mungu. Aina hizi tu za vitendo ndizo zinazoweza kuitwa kuingia katika uhalisi wa maneno Yake. Ikiwa una uwezo wa kuingia katika uhalisi huu, basi una ukweli. Huu ndio mwanzo wa kuingia katika uhalisi; lazima kwanza ufanye mazoezi haya na ni baada tu ya hayo ndio utakuwa na uwezo wa kuingia katika hali halisi za kina zaidi. Fikiria jinsi ya kushika amri na jinsi ya kuwa mwaminifu mbele ya Mungu. Usifikiri kila muda kuhusu wakati utakapoweza kuingia katika ufalme—ikiwa tabia yako haibadiliki, chochote unachokifikiria kitakuwa bure! Ili kuingia katika uhalisi wa maneno ya Mungu, lazima kwanza uweze kufanya mawazo yako na fikira zote ziwe kwa ajili ya Mungu—hili ni hitaji la msingi zaidi.

Kuna watu wengi ambao sasa wako katikati ya majaribio; hawaelewi kazi ya Mungu. Lakini Nakwambia—ikiwa huielewi, ni vyema usihukumu. Labda kutakuwa na siku moja wakati ukweli utajulikana na kisha utaujua. Kutohukumu kutakuwa na manufaa kwako, lakini huwezi kusubiri tu bila kuonyesha hisia. Lazima utafute kuingia ndani kwa matendo—huyu tu ndiye mtu anayeingia kwa vitendo. Kwa sababu ya uasi wao, watu daima wanaendeleza mawazo kuhusu Mungu wa vitendo. Hii inahitaji watu wote kujifunza jinsi ya kuwa watiifu kwa sababu Mungu wa vitendo ni jaribio kubwa kwa wanadamu. Ikiwa huwezi kusimama imara, basi kila kitu kimekamiliwa; kama huna ufahamu wa utendaji wa Mungu wa vitendo, huwezi kukamilishwa na Mungu. Hatua muhimu katika ikiwa watu wanaweza kufanywa kuwa kamili au sio ni kuelewa uzoefu wa Mungu. Uzoefu wa Mungu mwenye mwili aliyekuja duniani ni jaribio kwa kila mtu. Ikiwa unaweza kusimama imara katika kipengele hiki basi wewe ni mtu anayemjua Mungu, na wewe ni mtu anayempenda kwa kweli. Ikiwa huwezi kusimama imara katika kipengele hiki, ikiwa unamwamini tu Roho na huwezi kuwa na imani kwa utendaji wa Mungu, basi bila kujali jinsi imani yako ilivyo kubwa kwa Mungu, haina maana. Ikiwa huwezi kumwamini Mungu anayeonekana, unaweza kuamini Roho wa Mungu? Je, hujaribu kumdanganya Mungu? Wewe si mtiifu kwa Mungu anayeonekana na Anayeshikika, kwa hivyo unaweza kumtii Roho? Roho haishikiki na haionekani, kwa hiyo wakati unasema kwamba unatii Roho wa Mungu, je, huzungumzi tu upuuzi? Cha msingi katika kushika amri ni kuwa na ufahamu wa Mungu wa vitendo. Mara tu ukiwa na ufahamu wa Mungu wa vitendo, utakuwa na uwezo wa kushika amri. Kuna vipengele viwili katika kuzishika: Kimoja ni kushikilia kiini kiini cha Roho Wake, na mbele ya Roho, kuwa na uwezo wa kukubali uchunguzi wa Roho; kingine ni kuwa na uwezo wa kuwa na ufahamu wa kweli wa mwili wenye mwili, na kufikia utii wa kweli. Ikiwa ni mbele ya mwili au mbele ya Roho, moyo wa kumtii na kumcha Mungu lazima udumishwe daima. Ni mtu wa aina hii pekee ndiye anayestahiki kukamilishwa. Ikiwa una ufahamu wa utendaji wa Mungu wa vitendo—yaani, kama umesimama imara katika jaribio hili—kisha hakuna kitu kitakuwa kikubwa sana kwako.

Watu wengine husema, “Amri ni rahisi kushika. Unahitaji tu kuja mbele ya Mungu, kusema kwa uwazi na kwa dhati bila kutumia mikono, na huku ni kushika amri.” Je, hiyo ni sawa? Kwa hivyo, ukifanya mambo machache bila Mungu kujua ambayo yanampinga, je, hilo linahesabika kama kushika amri? Lazima uwe na ufahamu wa kina kuhusu kushika amri kunajumuisha nini. Linahusiana na ikiwa una ufahamu wa kweli wa utendaji wa Mungu au la; ikiwa una uelewa wa kutenda, na hujikwai na kuanguka katika jaribio hili, hili linahesabika kama wewe kuwa na ushahidi wa nguvu. Kuwa na ushahidi mkuu kwa Mungu hasa kunahusiana na ikiwa una ufahamu wa Mungu wa vitendo au la, na ikiwa unaweza au huwezi kutii mbele ya mtu huyu ambaye ni wa kawaida na kutii mpaka hata kifo. Ikiwa unamshuhudia Mungu kwa kweli kupitia

utii huu, hiyo inamaanisha kuwa umepatwa na Mungu. Kuwa na uwezo wa kutii mpaka kifo, na kuwa bila malalamiko mbele Yake, kutohukumu, kutokashifu, kutokuwa na mawazo, na kutokuwa na makusudi mengine—kwa njia hii Mungu atapata utukufu. Utiifu mbele ya mtu wa kawaida ambaye anadharauliwa na mwanadamu na kuwa na uwezo wa kutii mpaka kifo bila mawazo yoyote—huu ni ushuhuda wa kweli. Uhakika ambao Mungu anataka watu waingie ndani ni kwamba unaweza kutii maneno Yake, unaweza kuweka maneno Yake katika matendo, kuweza kuinama mbele ya Mungu wa vitendo na kujua upotovu wako mwenyewe, kuweza kufungua moyo wako mbele Yake, na mwishowe kupatwa na Yeye kupitia maneno haya Yake. Mungu hupata utukufu wakati maneno haya yanakushinda na kukufanya uwe mtiifu kikamilifu Kwake; kwa njia hii Anamwaibisha Shetani na kukamilisha kazi Yake. Wakati huna mawazo yoyote ya utendaji wa Mungu mwenye mwili, yaani, unaposimama imara katika jaribio hili, basi wewe huwa na ushuhuda mzuri. Ikiwa kuna siku ambayo uko na uelewa mkamilifu juu ya Mungu wa matendo na unaweza kutii mpaka kifo kama Petro, utapatwa na Mungu, na kukamilishwa na Yeye. Kile ambacho Mungu hufanya ambacho hakilingani na mawazo yako ni jaribio kwako. Ikiwa kingelingana na mawazo yako, hakingekuhitaji kuteseka au kusafishwa. Ni kwa sababu kazi Yake ni ya vitendo sana na kwamba hailingani na mawazo yako ndiyo inakuhitaji kuyaachilia mawazo yako. Hii ndiyo sababu ni jaribio kwako. Ni kwa sababu ya utendaji wa Mungu ndiyo maana watu wote wako katikati ya majaribio; kazi Yake ni ya vitendo, siyo ya kawaida. Kwa kuelewa kikamilifu maneno Yake ya vitendo, matamshi Yake ya vitendo bila mawazo yoyote, na kuwa na uwezo wa kumpenda kwa kweli zaidi ndivyo kazi Yake ilivyo ya vitendo zaidi, utapatwa na Yeye. Kundi la watu ambao Mungu atapata ni wale wanaomjua Mungu, yaani, ambao wanajua utendaji Wake, na hata zaidi ni wale wanaoweza kutii kazi ya vitendo ya Mungu.

Wakati wa Mungu akiwa ndani ya mwili, utii Anaohitaji kwa watu sio ule ambao watu wanafikiri—kutohukumu au kutopinga. Badala yake, Anahitaji kwamba watu wafanye maneno Yake kuwa kanuni yao ya maisha na msingi wa kuendelea kuishi kwao, kwamba wanaweka kikamilifu kiini cha maneno Yake katika matendo, na kwamba wanayaridhisha kabisa mapenzi Yake. Kipengele kimoja cha kuhitaji watu kumtii Mungu mwenye mwili kinahusu kuweka maneno Yake katika matendo, huku kipengele kingine kinarejelea kuwa na uwezo wa kutii ukawaida na utendaji Wake. Haya yote mawili lazima yawe bila shaka. Wale ambao wanaweza kutimiza vipengele hivi viwili ni wale wote ambao wana moyo wa upendo wa kweli kwa Mungu. Wote ni watu ambao wamepatwa na Mungu, na wote wanampenda Mungu kama wanavyopenda maisha yao wenyewe. Mungu mwenye mwili ana ubinadamu wa kawaida na wa utendaji katika kazi Yake. Kwa njia hii, gamba Lake la nje la ubinadamu wa kawaida na wa utendaji linakuwa jaribio kubwa kwa watu; linakuwa tatizo lao kubwa. Hata hivyo, ukawaida na utendaji wa

Mungu hauwezi kuepukwa. Alijaribu kila kitu ili kupata suluhisho lakini hatimaye hakuweza kujiondoa Mwenyewe kutoka kwenye gamba la nje la ubinadamu Wake wa kawaida kwa sababu, hata hivyo, Yeye ni Mungu aliyekuwa mwili, si Mungu wa Roho aliye mbinguni. Yeye si Mungu ambaye watu hawawezi kumuona, lakini Mungu aliyevaa gamba la kiumbe mmoja. Katika hili, kujiondoa Mwenyewe kutoka katika gamba la ubinadamu Wake wa kawaida bila shaka hakuwezi kuwa rahisi. Kwa hivyo bila kujali chochote, bado Yeye hufanya kazi ambayo Yeye hutaka kufanya kutoka kwa mtazamo wa mwili. Kazi hii ni maonyesho ya Mungu wa kawaida na wa matendo, kwa hivyo inawezekanaje kuwa sawa kwa watu kutotii? Ni nini duniani ambacho watu wanaweza kufanya kuhusu matendo ya Mungu? Anafanya chochote Anachotaka kufanya; chochote Anachofurahia kiko jinsi kilivyo. Ikiwa watu hawatii, wanaweza kuwa na mpango gani mwingine thabiti? Hadi sasa, bado ni utiifu tu ambao unaweza kuwaokoa watu; hakuna mawazo mengine ya ujanja. Ikiwa Mungu anataka kuwajaribu watu, wanaweza kufanya nini kuhusu hilo? Lakini yote haya si wazo la Mungu wa mbinguni; ni wazo la Mungu mwenye mwili. Anataka kufanya hili, hivyo hakuna mtu anayeweza kulibadilisha. Mungu aliye mbinguni haingilii kati kile Anachofanya, kwa hivyo watu hawapaswi kumtii hata zaidi? Ingawa Yeye ni wa matendo na wa kawaida, Yeye ni Mungu aliyekuwa mwili kikamilifu. Kulingana na mawazo Yake mwenyewe, Anafanya chochote Anachotaka. Mungu aliye mbinguni Amemkabidhi Yeye kazi zote; lazima utii chochote Anachofanya. Ingawa Ana ubinadamu na Yeye ni wa kawaida sana, yote haya ni yale ambayo Amepanga kwa makusudi, kwa hivyo watu wanaweza kumtazamaje, macho wazi kwa kutokubali? Anataka kuwa wa kawaida, kwa hivyo Yeye ni wa kawaida. Anataka kuishi ndani ya ubinadamu, hivyo Anaishi ndani ya ubinadamu. Anataka kuishi ndani ya uungu, hivyo anaishi ndani ya uungu. Watu wanaweza kuona hilo jinsi wanavyotaka. Mungu daima Atakuwa Mungu na watu daima watakuwa watu. Kiini Chake hakiwezi kukataliwa kwa sababu ya maelezo madogo, wala Hawezi kusukumwa nje ya “nafsi” ya Mungu kwa sababu ya kitu kidogo. Watu wana uhuru wa binadamu, na Mungu ana hadhi ya Mungu; haya hayaingiliani. Je, watu hawawezi kumpa Mungu uhuru kidogo? Je, hawawezi kumvumilia Mungu kuwa wa kawaida zaidi? Usiwe makini sana na Mungu! Kila mtu anapaswa kuwa na uvumilivu kwa kila mmoja; basi si kila kitu kitakuwa kimesuluhishwa? Je, bado kungekuwa na kufarakana kokote? Ikiwa mtu hawezi kuvumilia kitu kidogo kama hicho, anawezaje hata kufikiria kuwa mtu mkarimu, mwanadamu wa kweli? Siye Mungu anayewapa wanadamu wakati mgumu, lakini ni wanadamu wanaompa Mungu wakati mgumu. Daima wanashughulikia vitu kwa kufanya kitu kidogo kionekane kikubwa—kwa kweli wao hufanya kitu kisicho cha maana kuwa kizito, na hiyo si lazima! Wakati Mungu anafanya kazi katika ubinadamu wa kawaida na wa matendo, kile Anachofanya si kazi ya wanadamu, bali ni kazi ya Mungu. Hata hivyo, watu hawaoni kiini cha kazi Yake—daima wanaona gamba la nje la ubinadamu Wake. Hawajaona kazi kubwa kama hiyo, lakini wanasisitiza kuona ubinadamu wa

kawaida wa Mungu na hawaachilii wazo hili. Je, hii inawezaje kuitwa kumtii Mungu? Mungu mbinguni sasa “amegeuka kuwa” Mungu duniani, na Mungu duniani sasa ni Mungu wa mbinguni. Haijalishi kama sura Yao ya nje ni sawa au jinsi kazi Yao ilivyo. Kwa ujumla, Yeye anayefanya kazi ya Mungu mwenyewe ni Mungu Mwenyewe. Lazima utii bila kujali ikiwa unataka au la—hiki si kitu ambacho unapata kuchagua! Mungu lazima atiiwe na watu, na watu lazima wamtii kabisa Mungu bila ya kujifanya hata kidogo.

Kikundi cha watu ambao Mungu mwenye mwili Anataka kuwapata leo ni wale wanaokubali mapenzi Yake. Watu wanahitaji tu kutii kazi Yake, sio daima kujishughulisha na mawazo ya Mungu aliye mbinguni, waishi ndani ya hali isiyo dhahiri, au kufanya mambo kuwa magumu kwa Mungu mwenye mwili. Wale ambao wanaweza kumtii ni wale wanaoyasikia kabisa maneno Yake na kutii mipango Yake. Watu hawa hawajali kamwe jinsi Mungu mbinguni alivyo kwa kweli au ni kazi ya aina gani Mungu wa mbinguni Anafanya sasa kwa wanadamu, lakini wao humpa Mungu aliye duniani mioyo yao kabisa na kuweka nafsi zao zote mbele Yake. Kamwe hawazingatii usalama wao wenyewe, wala hawalalamiki kamwe juu ya ukawaida na utendaji wa Mungu katika mwili. Wale wanaomtii Mungu katika mwili wanaweza kukamilishwa na Yeye. Wale wanaomwamini Mungu mbinguni hawatapata kitu. Hii ni kwa sababu si Mungu mbinguni, lakini ni Mungu hapa duniani ndiye Anayetoa ahadi na baraka juu ya watu. Watu hawapaswi daima kumtukuza Mungu aliye mbinguni na kumwona Mungu duniani kama mtu wa wastani. Hii si haki. Mungu mbinguni ni mkuu na wa ajabu na mwenye hekima ya ajabu, lakini hii haipo kabisa. Mungu duniani ni wa wastani sana na asiye na maana; Yeye pia ni wa kawaida sana. Hana mawazo ya ajabu au vitendo vya kimiujiza. Anatenda tu na kuongea kwa njia ya kawaida na ya matendo. Ingawa Hazungumzi kwa njia ya ngurumo au kuita upepo na mvua, Yeye kwa kweli ni mwili wa Mungu aliye mbinguni, na kwa kweli ni Mungu anayeishi kati ya wanadamu. Watu hawapaswi kumtukuza yule wanayeweza kumwelewa na ambaye analingana na mawazo yao wenyewe kama Mungu, au kumwona Yeye ambaye hawawezi kumkubali na kabisa hawawezi kufikiria kama wa chini. Yote haya ni uasi wa watu; yote ni chanzo cha upinzani wa wanadamu kwa Mungu.

Wale Wanaopaswa Kukamilishwa Lazima Wapitie Usafishaji

Kama unamwamini Mungu, basi ni lazima umtii Mungu, uweke ukweli katika vitendo na utimize wajibu wako wote. Zaidi ya hayo, ni lazima uelewe mambo unayopaswa kupitia. Ikiwa unapitia tu kushughulikiwa, kufundishwa nidhamu na kuhukumiwa, kama wewe unaweza tu kumfurahia Mungu lakini usalie usiyeweza kuhisi wakati Mungu anakufundisha nidhamu au kukushughulikia—hili halikubaliki. Labda katika wakati huu wa usafishaji, unaweza kushikilia msimamo wako, bali hili bado halitoshi; ni lazima bado uendeleo kusonga mbele. Funzo la

kumpenda Mungu halikomi kamwe na halina mwisho. Watu huona kumwamini Mungu kama jambo lililo rahisi mno, lakini mara tu wanapopata uzoefu kiasi wa vitendo, wao kisha hutambua kwamba imani katika Mungu si rahisi kama watu wanavyofikiria. Wakati Mungu anafanya kazi ili kumsafisha mwanadamu, mwanadamu huteseka. Kadiri usafishaji wa mtu ulivyo mkubwa, ndivyo upendo wake kwa Mungu utakavyokuwa mkubwa zaidi na ndivyo nguvu za Mungu zitakavyofichuliwa zaidi kwake. Kinyume chake, kadiri mtu apokeavyo usafishaji mdogo zaidi, ndivyo upendo wake kwa Mungu utakavyokuwa kwa kiwango kidogo zaidi, na ndivyo nguvu za Mungu zitakavyofichuliwa kwake kwa kiwango kidogo zaidi. Kadiri usafishaji na uchungu wa mtu kama huyo ulivyo mkubwa na kadiri anavyopitia mateso mengi zaidi, ndivyo upendo wake kwa Mungu utakavyokuwa, ndivyo imani yake kwa Mungu itakavyokuwa ya kweli zaidi, na ndivyo maarifa yake ya Mungu yatakavyokuwa ya kina zaidi. Katika matukio unayopitia, utawaona watu wanaoteseka sana wanapokuwa wakisafishwa, wanaoshughulikiwa na kufundishwa nidhamu sana, na utaona kwamba ni watu hao ndio walio na upendo mkubwa kwa Mungu na maarifa ya kina na elekevu ya Mungu. Wale ambao hawajapitia kushughulikiwa wanayo maarifa ya juu juu tu, na wao wanaweza tu kusema: “Mungu ni mzuri sana, Yeye huwapa watu neema ili waweze kumfurahia Yeye.” Kama watu wamepitia kushughulikiwa na kufundishwa nidhamu, basi hao wanaweza kuzungumza kuhusu maarifa ya kweli ya Mungu. Hivyo kazi ya Mungu katika mwanadamu ilivyo ya ajabu zaidi, ndivyo ilivyo ya thamani zaidi na ni muhimu zaidi. Kadiri inavyokosa kupenyeza kwako zaidi na kadiri isivyolingana na mawazo yako, ndivyo kazi ya Mungu inavyoweza kukushinda, kukupata, na kukufanya mkamilifu. Umuhimu wa kazi ya Mungu ni mkubwa ulioje! Kama Mungu hangemsafisha mwanadamu kwa njia hii, kama Hangefanya kazi kulingana na njia hii, basi kazi Yake haingekuwa na ufanisi na ingekuwa isiyo na maana. Ilisemwa hapo awali kwamba Mungu angelichagua na kulipata kundi hili na kuwakamilisha katika siku za mwisho; hili lina umuhimu mkubwa sana. Kadiri kazi Anayofanya ndani yenu ilivyo kuu, ndivyo upendo wenu kwa Mungu ulivyo mkubwa na safi. Kadiri kazi ya Mungu ilivyo kuu zaidi, ndivyo mwanadamu anavyoweza kuelewa kitu kuhusu hekima Yake na ndivyo maarifa ya mwanadamu Kwake yalivyo ya kina zaidi. Katika siku za mwisho, miaka elfu sita ya mpango wa Mungu wa usimamizi itafika kikomo. Je, kweli inaweza kufika mwisho kwa urahisi? Baada ya Yeye kuwashinda wanadamu, je, kazi Yake itakuwa imefika mwisho? Je, inaweza kuwa rahisi vile? Watu kweli hufikiria kwamba ni rahisi hivi, lakini kile ambacho Mungu hufanya si rahisi vile. Bila kujali ni sehemu gani ya kazi ya Mungu unayojali kutaja, yote ni isiyoeleweka kwa mwanadamu. Ikiwa ungeweza kuifahamu, basi kazi ya Mungu ingekuwa isiyo na maana au thamani. Kazi inayofanywa na Mungu ni isiyoeleweka; ni kinyume kabisa na mawazo yako, na kadiri isivyopatana na mawazo yako, ndivyo inavyoonyesha zaidi kwamba kazi ya Mungu ni ya maana; kama ingekuwa inalingana na mawazo yako, basi ingekuwa isiyo maana. Leo, unahisi kwamba kazi ya Mungu ni

ya ajabu sana, na kadiri unavyohisi kuwa ni ya ajabu, ndivyo unahisi kwamba Mungu ni asiyeeleweka, na kuona jinsi matendo ya Mungu yalivyo makubwa. Kama Angefanya tu kazi fulani ya juu juu ya kutimiza wajibu kumshinda mwanadamu na Asifanye chochote zaidi baadaye, basi mwanadamu hangeweza kuona umuhimu wa kazi ya Mungu. Ingawa unapokea usafishaji kidogo sasa, ni wa faida kubwa sana kwa ukuaji wako katika maisha; hivyo ni jambo linalohitajika sana wewe kupitia ugumu wa aina hiyo. Leo, unapokea usafishaji kidogo, lakini baadaye utaweza kwa kweli kuyaona matendo ya Mungu, na hatimaye utasema: “Matendo ya Mungu ni ya ajabu mno!” Haya ndiyo yatakuwa maneno moyoni mwako. Baada ya kupitia usafishaji wa Mungu kwa muda (majaribu ya watendaji huduma na wakati wa kuadibu), baadhi ya watu hatimaye walisema: “Kuamini katika Mungu ni jambo gumu kweli!” Ukweli kwamba wao hutumia maneno “jambo gumu kweli”, unaonyesha kwamba matendo ya Mungu ni yasiyoeleweka, kuwa kazi ya Mungu ni yenye umuhimu na thamani kubwa, na kwamba kazi Yake ni yenye kustahili sana kuthaminiwa na mwanadamu. Ikiwa, baada ya Mimi kufanya kazi nyingi hivi, hukuwa na maarifa hata kidogo, basi kazi Yangu ingeweza kuwa na thamani bado? Itakufanya useme: “Huduma kwa Mungu ni ngumu kweli, matendo ya Mungu ni ya ajabu mno, na Mungu kweli ni mwenye hekima! Mungu ni mwenye kupendeza kweli!” Kama, baada ya kupitia kipindi cha uzoefu, una uwezo wa kusema maneno kama haya, basi hii inathibitisha kuwa umepata kazi ya Mungu ndani yako. Siku moja, ukiwa unaeneza injili ughaibuni na mtu akuulize: “Imani yako katika Mungu inaendeleaje?” Utaweza kusema: “Matendo ya Mungu ni ya ajabu kweli!” Mtu huyo atahisi kwamba maneno yako yanazungumza kuhusu matukio halisi uliyopitia. Huku kweli ni kutoa ushahidi. Utasema kuwa kazi ya Mungu imejaa hekima, na kazi Yake ndani yako imekushawishi kwa kweli na kuushinda moyo wako. Wewe daima utampenda kwa maana Yeye anastahili zaidi upendo wa wanadamu! Kama unaweza kuzungumza kwa vitu hivi, basi unaweza kuigusa mioyo ya watu. Haya yote ni kutoa ushahidi. Kama unaweza kuwa shahidi wa ajabu, kuwagusa watu hadi watoe machozi, hiyo inaonyesha kwamba kwa kweli wewe ni mmoja anayempenda Mungu, kwa sababu unaweza kushuhudia kuhusu kumpenda Mungu, na kupitia kwako, matendo ya Mungu yanaweza kushuhudiwa. Kupitia ushuhuda wako, wengine wanafanywa watafute kazi ya Mungu, wapitie kazi ya Mungu, na katika mazingira yoyote wanayopitia, wataweza kusimama imara. Hii pekee ndiyo njia ya kweli ya kuwa shahidi, na hili hasa ndilo linalohitajika kutoka kwako sasa. Unafaa kuona kwamba kazi ya Mungu ni muhimu sana na inastahili kuthaminiwa na watu, kwamba Mungu ni wa thamani mno na mwenye Mengi, Hawezi tu kusema, lakini pia Anaweza kutoa uamuzi juu ya watu, kusafisha mioyo yao, kuwaletea starehe, kuwapata, kuwashinda, na kuwakamilisha. Kutoka katika kupitia kwako utaona kwamba Mungu ni mwenye kupendwa sana. Hivyo unampenda Mungu kiasi gani sasa? Je, unaweza kweli kusema mambo haya kutoka moyoni mwako? Wakati unaweza kuonyesha maneno haya kutoka kwenye kina cha moyo wako, basi utaweza kuwa na ushuhuda.

Mara tu uzoefu wako unapofikia kiwango hiki utakuwa na uwezo wa kuwa shahidi wa Mungu, na utakuwa umestahili. Kama huwezi kufika kiwango hiki katika uzoefu wako, basi wewe bado utakuwa mbali sana. Ni jambo la kawaida kwa watu kuonyesha udhaifu katika mchakato wa usafishaji, lakini baada ya usafishaji unapaswa kuweza kusema: “Mungu ni mwenye hekima sana katika kazi Yake!” Kama wewe kweli unaweza kufikia ufahamu wa vitendo wa maneno haya, basi kitakuwa kitu unachokithamani, na uzoefu wako utakuwa wa thamani.

Je, ni nini unachopaswa kufuatilia sasa? Iwapo unaweza kushuhudia kazi ya Mungu au la, iwapo unaweza kuwa ushuhuda na udhihirisho wa Mungu au la, na iwapo unastahili kutumiwa na Yeye au la—hivi ndivyo vitu unavyopaswa kutafuta. Ni kiasi gani cha kazi ambacho Mungu hakika amefanya kwako? Ni kiasi gani ambacho umeona, ni kiasi gani ambacho umegusa? Umepitia kiasi gani, na kuonja kiasi gani? Bila kujali iwapo Mungu amekujaribu, kukushughulikia, au kukuadhibu, matendo Yake na kazi Yake vimetekelezwa juu yako. Lakini kama muumini katika Mungu na kama mtu ambaye ana nia ya kufuatilia kukamilishwa na Yeye, je, unaweza kushuhudia kazi ya Mungu kwa msingi wa uzoefu wako wa vitendo? Je, Je, unaweza kuishi kwa kudhihirisha neno la Mungu kupitia kwa uzoefu wako wa vitendo? Je, unaweza kuwakimu wengine kupitia uzoefu wako mwenyewe wa vitendo, na kutumia maisha yako yote kushuhudia kazi ya Mungu? Ili kushuhudia kazi ya Mungu, lazima utegemee uzoefu na maarifa yako, na gharama ambayo umelipa. Unaweza kuyaridhisha mapenzi Yake kwa njia hii pekee. Je, wewe ni mtu ambaye hushuhudia kazi ya Mungu? Je, una matamano haya? Kama unaweza kulishuhudia jina Lake, na hata zaidi, kazi Yake, na kama unaweza kuishi kwa kudhihirisha sura ambayo Yeye anataka kutoka kwa watu Wake, basi wewe ni shahidi wa Mungu. Je, unashuhudia kwa ajili ya Mungu vipi kwa hakika? Unafanya hivyo kwa kutafuta na kuwa na hamu sana ya kuishi kwa kulidhihirisha neno la Mungu na, kwa kuwa na shahidi kwa maneno yako, kuwaruhusu watu wajue kazi Yake na kuona matendo Yake. Kama kweli unatafuta yote haya, basi Mungu atakukamilisha. Ikiwa yote unayotafuta ni kukamilishwa na Mungu na kubarikiwa mwishoni kabisa, basi mtazamo wa imani yako katika Mungu si safi. Unapaswa kuwa ukifuatilia jinsi ya kuona matendo ya Mungu katika maisha ya kweli, jinsi ya kumridhisha Yeye Anapokufichulia mapenzi Yake, na kutafuta jinsi unavyopaswa kushuhudia maajabu na hekima Yake, na jinsi ya kushuhudia jinsi Anavyokufundisha nidhamu na kukushughulikia. Haya yote ni mambo unavyopaswa kuwa ukiyatafakari sasa. Kama upendo wako kwa Mungu ni ili tu uweze kushiriki katika utukufu wa Mungu baada ya Yeye kukukamilisha, basi bado hautoshi na hauwezi kukidhi mahitaji ya Mungu. Unahitaji kuwa na uwezo wa kushuhudia kazi ya Mungu, kutosheleza mahitaji Yake, na kuwa na uzoefu wa kazi ambayo Amefanya kwa watu kwa njia ya utendaji. Iwe ni uchungu, majonzi, au huzuni, lazima upitie vitu hivi vyote katika kutenda kwako. Vitu hivi vinanuiwa kukukamilisha kama Yule

anayemshuhudia Mungu. Ni nini hasa kinachokushurutisha sasa kuteseka na kutafuta kukamilishwa? Je, mateso yako ya sasa kweli ni kwa ajili ya kumpenda Mungu na kumshuhudia? Ama ni kwa ajili ya Baraka za mwili na matarajio na kudura yako ya baadaye? Dhamira zako zote, nia, na malengo unayofuatilia lazima yarekebishwe na hayawezi kuongozwa na mapenzi yako mwenyewe. Kama mtu mmoja anatafuta ukamilifu ili apokee baraka na kutawala mamlakani, wakati mtu mwingine anafuatilia ukamilifu ili amridhishe Mungu, awe na ushuhuda wa vitendo wa kazi ya Mungu, je, ni ipi kati ya njia hizi mbili za ufuatiliaji ndiyo ungechagua? Ikiwa utachagua ya kwanza, basi utakuwa mbali sana na viwango vya Mungu. Nilisema wakati mmoja kwamba matendo Yangu yatajulikana wazi katika ulimwengu wote na kwamba Ningetawala kama Mfalme katika ulimwengu. Kwa upande mwingine, kilichoaminiwa kwenu ni kuenda kushuhudia kazi ya Mungu, sio kuwa wafalme na kuonekana ulimwenguni wote. Hebu matendo ya Mungu yajazee ulimwengu na anga. Hebu kila mtu ayaone na ayakiri. Maneno haya yanasemwa kuhusiana na Mungu Mwenyewe, na kile ambacho wanadamu wanapaswa kufanya ni kutoa ushuhuda kwa ajili ya Mungu. Je, unajua kiasi gani kuhusu Mungu sasa? Je, unaweza kutoa ushuhuda kwa Mungu kiasi gani? Je, ni lengo gani la Mungu kumkamilisha mwanadamu? Mara baada ya kuelewa mapenzi ya Mungu, je, unapaswa kuonyeshaje kujali kuelekea mapenzi Yake? Kama uko tayari kukamilishwa na uko tayari kushuhudia kazi ya Mungu kupitia kile unachoishi kwa kudhihirisha, kama una hii nguvu ya msukumo, basi hakuna lililo gumu sana. Wanachohitaji watu sasa ni imani. Kama una hii nguvu ya msukumo, basi ni rahisi kuachilia chochote chenye uhasi, cha kukaa tu, uvivu na mawazo ya mwili, falsafa za kuishi, tabia ya uasi, hisia, na mengineyo.

Wakati wanapitia majaribu, ni kawaida kwa watu kuwa dhaifu, au kuwa na uhasi ndani yao, au kukosa uwazi juu ya mapenzi ya Mungu au njia yao ya kutenda. Lakini katika hali yoyote, lazima uwe na imani katika kazi ya Mungu, na usimkane Mungu, kama tu Ayubu. Ingawa Ayubu alikuwa dhaifu na aliilaani siku yake ya kuzaliwa, yeye hakukana kwamba vitu vyote katika maisha ya binadamu vilikuwa vimetolewa na Yehova, na kwamba Yehova pia Ndiye anayeyachukua vyote. Haijalishi jinsi alivyojaribiwa, alidumisha imani hii. Katika kupitia kwako, haijalishi ni usafishaji gani unaopitia katika maneno ya Mungu, kile Mungu anahitaji kutoka kwa wanadamu kwa ufupi ni imani yao na upendo wao Kwake. Anachokamilisha kwa kufanya kazi kwa njia hii ni imani, upendo na matarajio ya watu. Mungu hufanya kazi ya ukamilisho kwa watu, nao hawawezi kuiona, hawawezi kuihisi; katika hali kama hizi imani yako inahitajika. Imani ya watu inahitajika wakati ambao kitu hakiwezi kuonekana kwa macho tu, na imani yako inahitajika wakati huwezi kuziachilia dhana zako mwenyewe. Wakati ambapo huna uwazi kuhusu kazi ya Mungu, kinachohitajika kutoka kwako ni kuwa na imani uchukue msimamo imara na kuwa shahidi. Wakati Ayubu alifikia hatua hii, Mungu alimwonekana na kuzungumza

naye. Yaani, ni kutoka ndani ya imani yako tu ndipo utaweza kumwona Mungu, na wakati una imani Mungu atakukamilisha. Bila imani, Hawezi kufanya hivyo. Mungu ataweka juu yako chochote ulicho na matumaini ya kupata. Kama huna imani, basi huwezi kukamilishwa na hutakuwa na uwezo wa kuona matendo ya Mungu, sembuse kudura Yake. Wakati una imani kwamba utaona matendo Yake katika uzoefu wako wa utendaji, basi Mungu atakuonekana, na Atakupa nuru na kuongoza kutoka ndani. Bila hiyo imani, Mungu hataweza kufanya hivyo. Kama umepoteza matumaini katika Mungu, utawezaje kupata uzoefu wa kazi Yake? Kwa hiyo, ni wakati tu una imani na huweki mashaka kumhusu Mungu, ni wakati una imani ya kweli Kwake tu bila kujali Anachokifanya ndipo Atakuangazia na kukupa nuru kupitia katika mapito yako, na ni hapo tu ndipo utaweza kuona matendo Yake. Mambo haya yote yanafanikishwa kupitia kwa imani. Imani huja kupitia tu usafishaji, na wakati hakuna usafishaji, imani haiwezi kukua. Je, neno hili “imani”, linarejelea nini? Imani ni kusadiki kwa kweli na moyo wa dhati ambao wanadamu wanapaswa kumiliki wakati wao hawawezi kuona au kugusa kitu, wakati kazi ya Mungu haiambatani na za binadamu, wakati inazidi uwezo wa binadamu. Hii ndiyo imani Ninayozungumzia. Watu wanahitaji imani katika nyakati za shida na usafishaji, na imani ni kitu kinachofuatwa na usafishaji; usafishaji na imani haviwezi kutenganishwa. Haijalishi jinsi Mungu anavyofanya kazi, na haijalishi mazingira uliyomo, unaweza kufuatilia maisha na kutafuta ukweli, na kutafuta maarifa ya kazi ya Mungu, na kuwa na ufahamu wa matendo Yake, na unaweza kutenda kulingana na ukweli. Kufanya hivi ndiko kuwa na imani ya kweli, na kufanya hivyo kunaonyesha kwamba hujapoteza imani katika Mungu. Unaweza tu kuwa na imani ya kweli katika Mungu ikiwa bado unaweza kuendelea kufuatilia ukweli kupitia ukiwa katika usafishaji, ikiwa unaweza kumpenda Mungu kwa kweli na huna na mashaka kumhusu Yeye, ikiwa bila kujali Anachokifanya bado unatenda ukweli kumridhisha Yeye, na ikiwa unaweza kutafuta kwa dhati mapenzi Yake na ujali mapenzi Yake. Zamani, wakati Mungu alisema kwamba ungetawala kama mfalme, ulimpenda, na wakati Alijionyesha hadharani kwako, ulimfuata. Lakini sasa Mungu amejificha, huwezi kumwona, na shida zimekuja—je, hapo unapoteza matumaini kwa Mungu? Hivyo, lazima ufuatilie uzima wakati wote na kutafuta kuyaridhisha mapenzi ya Mungu. Hii inaitwa imani ya kweli, na huu ndio aina ya upendo ulio wa kweli na mzuri zaidi.

Hapo zamani, watu wote walikuja mbele za Mungu kufanya maazimio yao na walisema: “Hata kama hakuna mtu mwingine anayempenda Mungu, ni lazima mimi nimpende.” Lakini sasa, usafishaji unakujia, na kwa sababu hili halilingani na fikira zako, hivyo unapoteza imani katika Mungu. Je, huu ni upendo wa kweli? Umesoma mara nyingi kuhusu matendo ya Ayubu—Je, umesahau kuyahusu? Upendo wa kweli unaweza tu kukua kutoka ndani ya imani. Unakuza upendo wa kweli kwa Mungu kupitia katika usafishaji unaopitia, na ni kupitia kwa imani yako

ndiyo unaweza kuyadhukuru mapenzi ya Mungu katika matukio yako ya vitendo, na pia ni kupitia kwa imani yako ndiyo unautelekeza mwili wako mwenyewe na kufuatilia uzima; hili ndilo watu wanapaswa kufanya. Ukifanya hivi, basi utaweza kuona matendo ya Mungu, lakini ukikosa imani, basi hutaweza kuona matendo ya Mungu au kuipitia kazi Yake. Iwapo unataka kutumika na kukamilishwa na Mungu, ni lazima umiliki kila kitu: uwe tayari kuteseka, imani, uvumilivu, utiifu na uwezo wa kupitia kazi ya Mungu, kufahamu mapenzi Yake kujali huzuni Yake, na kadhalika. Kumkamilisha mtu si rahisi, na kila kisa cha usafishaji unachopitia kinahitaji imani na upendo wako. Kama unataka kukamilishwa na Mungu, haitoshi kukimbia tu mbele kwenye njia, wala haitoshi kujitumia tu kwa ajili ya Mungu. Ni lazima umiliki mambo mengi ili uweze kuwa mtu ambaye anakamilishwa na Mungu. Unapokabiliwa na mateso ni lazima uweze kuweka kando masilahi ya mwili na usifanye malalamiko dhidi ya Mungu. Wakati Mungu anajificha kutoka kwako, ni lazima uweze kuwa na imani ya kumfuata Yeye, kudumisha upendo wako wa awali bila kuuruhusu ufifie au kutoweka. Haijalishi anachofanya Mungu, ni lazima utii mpango Wake na uwe tayari kuulaani mwili wako mwenyewe badala ya kulalamika dhidi Yake. Wakati unakabiliwa na majaribu, lazima umridhishe Mungu, ingawa unaweza kulia kwa uchungu au uhisi kusita kuhusu kuacha kitu unachopenda. Huu tu ndio upendo wa kweli na imani. Haijalishi kimo chako halisi ni kipi, ni lazima kwanza umiliki nia ya kupitia ugumu na imani ya kweli, na ni pia lazima uwe na nia ya kuutelekeza mwili. Unapaswa kuwa tayari kuvumilia ugumu wa kibinafasi na kupata hasara kwa maslahi yako binafsi ili kuridhisha mapenzi ya Mungu. Lazima pia uwe na uwezo wa kuhusi majuto kujihusu moyoni mwako: Hapo zamani, hukuweza kumridhisha Mungu, na sasa unaweza kujuta mwenyewe. Ni lazima usipungukiwe katika yoyote ya hali hizi—Ni kupitia katika vitu hivi ndiyo Mungu atakukamilisha. Usipoweza kufikia viwango hivi, basi huwezi kukamilishwa.

Mtu anayemtumikia Mungu lazima asijue jinsi ya kuteseka kwa ajili Yake; zaidi ya hayo, anapaswa kuelewa kwamba kusudi la kuamini katika Mungu ni kwa ajili ya kufuatilia kumpenda Mungu. Mungu hukutumia si kwa sababu tu ya kukusafisha au kwa sababu ya kukufanya uteseke, lakini badala yake ni Yeye hukutumia ili uweze kujua matendo Yake, kujua umuhimu halisi wa maisha ya binadamu, na hasa, ili uweze kujua kwamba kumtumikia Mungu si kazi rahisi. Kupata uzoefu wa kazi ya Mungu hakuhusu kufurahia neema Yake, bali kuhusu kuteseka kwa sababu ya upendo wako Kwake. Kwa kuwa unafurahia neema ya Mungu, lazima pia ufurahie kuadibu Kwake; lazima upitie haya yote. Unaweza kupata uzoefu wa nuru ya Mungu ndani yako, na unaweza pia kupitia jinsi Anavyokushughulikia na Anavyokuhukumu. Kwa njia hii, uzoefu wako utakuwa mkamilifu. Mungu ametelekeza kazi Yake ya hukumu na kuadibu kwako. Neno la Mungu limekushughulikia, lakini si hilo yu; pia limekupa nuru, na kukuangazia. Wakati wewe ni hasi na dhaifu, Mungu ana wasiwasi kwa ajili yako. Hizi kazi zote ni za

kukufahamisha kwamba kila kitu kuhusu mwanadamu kimo katika udhibiti wa Mungu. Unaweza kufikiri kwamba kuamini katika Mungu ni kuhusu mateso, au kumfanyia mambo ya kila aina; unaweza kufikiri kwamba sababu ya kumwamini Mungu ni ili mwili wako uwe na amani, au ili kwamba kila kitu maishani mwako kiende vizuri, au ili kwamba uweze kuwa na raha na utulivu katika kila kitu. Hata hivyo, hakuna kati ya haya ambayo watu wanapaswa kuhusisha na imani yao katika Mungu. Ukiamini kwa ajili ya sababu hizi, basi mtazamo wako si sahihi na haiwezekani kabisa wewe kukamilishwa. Matendo ya Mungu, tabia ya Mungu ya haki, hekima Yake, maneno Yake, na maajabu Yake na kutoeleweka kwa kina Kwake yote ni mambo ambayo watu wanapaswa kuelewa. Kuwa na ufahamu huu, unapaswa kuutumia kuondoa moyoni mwako madai, matumaini na fikiza za kibinafsi. Ni kwa kuondoa mambo haya tu ndiyo unaweza kukidhi masharti yanayotakiwa na Mungu, na ni kwa kufanua hivi tu ndiyo unaweza kuwa na uzima na kumridhisha Mungu. Kusudi la kumwamini Mungu ni ili kumridhisha na kuishi kwa kudhihirisha tabia ambayo Yeye anahitaji, ili matendo na utukufu Wake viweze kudhihirishwa kupitia kundi hili la watu wasiostahili. Huu ndio mtazamo sahihi wa kuamini katika Mungu, na hili pia ndilo lengo unalopaswa kutafuta. Unapaswa kuwa na mtazamo sahihi kuhusu kuamini katika Mungu na unapaswa kutafuta kupata maneno ya Mungu. Unahitaji kula na kunywa maneno ya Mungu na lazima uwe na uwezo wa kuishi kwa kudhihirisha ukweli, na hasa lazima uweze kuona matendo Yake ya vitendo, matendo Yake ya ajabu kotekote katika ulimwengu mzima, pamoja na kazi ya vitendo Yeye hufanya katika mwili. Kupitia katika uzoefu wao wa vitendo, watu wanaweza kufahamu ni jinsi gani hasa Mungu hufanya kazi Yake kwao na mapenzi Yake kwao ni yapi. Kusudi la haya yote ni ili kuondoa tabia potovu ya kishetani ya watu. Baada ya kuondoa uchafu na udhalimu wote ulio ndani mwako, na baada ya kuondoa nia zako mbaya, na baada ya kukuza imani ya kweli kwa Mungu—ni kwa kuwa na imani ya kweli tu ndiyo unaweza kumpenda Mungu kweli. Unaweza tu kweli kumpenda Mungu kwa msingi wa imani yako Kwake. Je, unaweza kufanikisha upendo wa kweli kwa Mungu bila kumwamini? Kwa kuwa unaamini katika Mungu, huwezi kukanganyika kuhusu jambo hilo. Baadhi ya watu hujawa na nguvu mara tu wanapoona kwamba imani katika Mungu itawaletea baraka, lakini kisha hupoteza nguvu zote mara tu wanapoona kwamba wanafaa kupitia kusafishwa. Je, huko ni kuamini katika Mungu? Mwishowe, lazima upate utiifu kamili na mzima mbele ya Mungu katika imani yako. Unaamini katika Mungu lakini bado una madai Kwake, una mawazo mengi ya kidini ambayo huwezi kuyapuuza, maslahi ya kibinafsi huwezi kuacha, na bado unatafuta baraka za mwili na unataka Mungu auokoe mwili wako, kuiokoa nafsi yako—hizi zote ni tabia za watu walio na mtazamo usio sahihi. Hata kama watu wenye imani za kidini wana imani katika Mungu, hawatafuti kubadilisha tabia zao na hawafuatilii maarifa ya Mungu, lakini badala yake wanatafuta tu masilahi ya miili yao. Wengi kati yenu wana imani ambazo ni za kikundi cha kusadiki kidini; hii siyo imani ya kweli katika Mungu. Kuamini katika Mungu, watu lazima

wamiliki moyo ulio tayari kuteseka kwa ajili Yake na radhi ya kujitoa wenyewe. Watu wasipokidhi haya masharti mawili, imani yao katika Mungu haihesabiki, na hawataweza kufanikisha mabadiliko katika tabia yao. Ni watu tu wanaotafuta ukweli kwa kweli, wanaotafuta maarifa ya Mungu, na kufuatilia maisha ndio wale ambao kweli wanaamini katika Mungu.

Wakati majaribu yanakujia, utaitumiaje kazi ya Mungu kushughulikia majaribu hayo? Je, utakuwa hasi au utaelewa jaribu na usafishaji wa Mungu wa mwanadamu kutoka kwa kipengele chema? Utapata faida gani kutoka kwa majaribu na usafishaji wa Mungu? Je, upendo wako kwa Mungu utaongezeka? Wakati unapitia usafishaji, je, utaweza kutumia majaribu ya Ayubu na ujishughulishe kwa ari na kazi ambayo Mungu anafanya ndani yako? Je, unaweza kuona jinsi Mungu anavyompima mwanadamu kwa njia ya majaribu ya Ayubu? Ni aina gani ya mvuto ambao majaribu ya Ayubu yanaweza kuleta kwako? Je, utakuwa tayari kuwa shahidi kwa Mungu katikati ya usafishaji wako, au utataka kuuridhisha mwili katika mazingira ya starehe? Mtazamo wako kuhusu imani kwa Mungu ni upi kwa kweli? Je, kweli ni kwa ajili Yake, na si kwa ajili ya mwili? Je, kweli una lengo ambalo unafuatilia katika kutafuta kwako? Je, uko tayari kupitia usafishaji ili uweze kufanywa mkamilifu na Mungu, au badala yake ungeona heri kuadibiwa na kulaaniwa na Mungu? Mtazamo wako juu ya suala la kuwa na ushuhuda wa Mungu? Watu wanapaswa kufanya nini katika mazingira fulani ili wamshuhudie Mungu kwa kweli? Kwa kuwa Mungu wa utendaji amefichua mengi sana kazi Yake ya hakika ndani yako, kwa nini siku zote una mawazo ya kuondoka? Je, imani yako katika Mungu ni kwa ajili ya Mungu? Kwa wengi wenu, imani yeny ni sehemu ya hesabu mnayofanya kwa niaba yenu wenyewe, kwa ajili ya ufuatiliaji wa faida zenu binafsi. Watu wachache sana wanaamini katika Mungu kwa ajili ya Mungu; je, huu sio ukaidi?

Kusudi la kazi ya usafishaji kimsingi ni ya kukamilisha imani ya watu. Mwishowe, kile kinachofanikishwa ni kwamba unataka kuondoka lakini, wakati huo huo, huwezi; baadhi ya watu bado wanaweza kuwa na imani hata wakati wanaondolewa hata chembe kidogo cha matumaini; na watu hawana tena tumaini kabisa kuhusu matarajio ya siku za zao za usoni. Ni katika wakati huu tu ndipo usafishaji wa Mungu utafikia kikomo. Mwanadamu bado hajafikia hatua ya kuelea kati ya maisha na kifo, na hajaonja mauti, hivyo mchakato wa usafishaji bado haujakamilika. Hata wale ambao walikuwa katika hatua ya watenda huduma hawakuwa wamesafishwa kabisa. Ayubu alipitia usafishaji mkali sana, na hakuwa na kitu cha kutegemea. Watu lazima wapitie usafishaji mpaka ile hatua ambayo hawana matumaini na kitu cha kutegemea—huu tu ndio usafishaji wa kweli. Wakati wa watenda huduma, ikiwa moyo wako daima ulikuwa umetulia mbele ya Mungu, na ikiwa pasipo kujali Alichofanya na pasipo kujali mapenzi Yake kwa ajili yako yalikuwa nini, wewe daima ulitii mipango Yake, basi mwishoni ungeelewa kila kitu ambacho Mungu alikuwa amefanya. Unapitia majaribu ya Ayubu, na wakati uo huo unapitiaa

majaribu ya Petro. Wakati Ayubu alijaribiwa, yeye alikuwa shahidi, na mwishowe, Yehova alidhihirishwa kwake. Ni baada tu ya kuwa shahidi ndipo alistahili kuona uso wa Mungu. Kwa nini inasemwa: “Mimi najificha kutoka nchi ya uchafu lakini Najionyesha kwa ufalme mtakatifu”? Hiyo ina maana kwamba wakati tu uko mtakatifu na kuwa shahidi ndipo unaweza kuwa na hadhi ya kuuona uso wa Mungu. Kama huwezi kuwa shahidi kwa ajili Yake, hauna hadhi ya kuuona uso Wake. Ukijiondoa au kufanya malalamiko kwa Mungu ukikabiliwa na usafishaji, hivyo ushindwe kuwa shahidi Wake na uwe kichekesho cha Shetani, basi hutapata sura ya Mungu. Kama wewe ni kama Ayubu, ambaye katikati ya majaribu aliulaani mwili wake na wala hakulalamika dhidi ya Mungu, na aliweza kuuchukia mwili wake bila kulalamika au kutenda dhambi kwa njia ya maneno yake, basi utakuwa shahidi. Unapopitia usafishaji kwa kiasi fulani na bado unaweza kuwa kama Ayubu, mtiifu kabisa mbele ya Mungu na bila mahitaji mengine Kwake au dhana zako mwenyewe, basi Mungu atakuonekana. Sasa Mungu hakuonekanii kwa sababu una nyingi za dhana zako mwenyewe, maoni binafsi, mawazo ya ubinafsi, mahitaji ya binafsi na maslahi ya kimwili, na wewe hustahili kuuona uso Wake. Kama ungempima Mungu, ungempima kupitia katika mawazo yako mwenyewe na, kwa kufanya hivyo, Angesulubishwa msalabani nawewe. Kama mambo mengi yanakuja kwako ambayo si sambamba na dhana zako lakini bado unaweza kuyaweka kando na kupata ufahamu wa matendo ya Mungu kutoka kwa mambo haya, na katikati ya usafishaji unadhihirisha moyo wako wa upendo kwa Mungu, basi huku ni kuwa shahidi. Kama nyumba yako ina amani, unafurahia starehe za mwili, hakuna mtu anayekutesa, na ndugu na dada zako katika kanisa wanakutii, je, unaweza kuonyesha moyo wako wa upendo kwa Mungu? Je, hali hii inaweza kukusafisha? Ni kwa kupitia katika usafishaji tu ndiyo upendo wako kwa Mungu unaweza kuonyeshwa, na ni kwa mambo yasiyo sambamba na fikira zako kutokea tu ndiyo unaweza kukamilishwa. Akitumia mambo mengi yasiyofaa na mabaya na kwa kutumia kila aina ya maonyesho ya Shetani—matendo yake, lawama yake, usumbufu wake na udanganyifu wake—Mungu hukuonyesha sura mbaya ya Shetani vizuri, na hivyo Anakamilisha uwezo wako wa kumbainisha Shetani, ili uweze kumchukua Shetani na uachane naye.

Uzoefu wako mwingi wa kushindwa, udhaifu, nyakati zako za uhasi, vyote vinaweza kusemekana kuwa majaribu ya Mungu. Hii ni kwa sababu kila kitu hutoka kwa Mungu, na mambo yote na matukio yako katika mikono Yake. Kama unashindwa au kama wewe ni dhaifu na unajikwaa, yote yako kwa Mungu na vipo katika mfumbato Wake. Kutoka kwa mtazamo wa Mungu, haya ni majaribu yako, na kama huwezi kutambua hivyo, yatageuka majaribu. Kuna aina mbili za hali ambazo watu wanapaswa kutambua: Moja inatoka kwa Roho Mtakatifu, na chanzo cha nyingine huenda ni Shetani. Moja ni hali ambamo Roho Mtakatifu anakuangazia na Anakuruhusu upate kujijua mwenyewe, kuchukia na kuhisi majuto kujihusu mwenyewe na

kuweza kuwa na upendo wa kweli kwa Mungu, kuweka moyo wako katika kumridhisha Yeye. Nyingine ni hali ambamo unajijua mwenyewe, lakini wewe ni hasi na dhaifu. Inaweza kusemwa pia kuwa hii ni hali ya usafishaji wa Mungu, na pia kuwa ni ushawishi wa Shetani. Ukitambua kuwa huu ni wokovu wa Mungu kwako na ukihisi kuwa wewe sasa ni mdeni Wake mkubwa, na kama kuanzia sasa utajaribu kulipa deni Lake na usianguke tena katika upotovu kama huo, kama utaweka juhudi katika kula na kunywa maneno Yake, na kama siku zote unajichukua kama anayekosa, na kuwa na moyo wa hamu, basi haya ni majaribu ya Mungu. Baada ya mateso kumalizika na wewe kwa mara nyingine tena unasonga mbele, Mungu bado atakuongoza, atakuangazia, atakupa nuru, na kukusitawisha. Lakini kama hilitambui na wewe ni hasi, kujiachilia tu kukata tamaa, kama unafikiri hivi, basi kishawishi cha Shetani kimekufikia. Wakati Ayubu alipitia majaribu, Mungu na Shetani walikuwa wanawekeana dau, na Mungu alimruhusu Shetani amtese Ayubu. Hata ingawa ilikuwa ni Mungu aliyekuwa anamjaribu Ayubu, hakika alikuwa ni Shetani ndiye aliyemjia. Kwa Shetani, ilikuwa ni kumjaribu Ayubu, lakini Ayubu alikuwa upande wa Mungu. Kama haingekuwa vile, basi Ayubu angeanguka katika kishawishi. Mara baada ya watu kuanguka katika kishawishi, wao huanguka katika hatari. Kupitia usafishaji inaweza kusemwa kuwa jaribu kutoka kwa Mungu, lakini kama hauko katika hali nzuri inaweza kusemwa kuwa kishawishi kutoka kwa Shetani. Kama hauko na uwazi juu ya maono, Shetani atakushutumu na kukuvuruga katiza mtazamo wa maono. Kabla ya kujua, utaanguka katika majaribu.

Kama hupitii kazi ya Mungu, basi kamwe hutaweza kufanywa mkamilifu. Katika uzoefu wako, lazima pia uingie katika maelezo. Kwa mfano, ni vitu vipi hukuongoza kukuza dhana na nia za kupita kiasi, na ni aina gani za matendo yanayofaa uliyo nayo kushughulikia matatizo haya? Kama unaweza kupitia kazi ya Mungu, hii ina maana kwamba una kimo. Kama unaonekana tu kuwa na nguvu, hiki si kimo halisi na hutaweza kusimama imara hata kidogo. Ni wakati tu unaweza kupitia kazi ya Mungu na uweze kuipitia na kuitafakari wakati wowote na mahali popote, wakati unaweza kuwaacha wachungaji na uishi peke yako ukimtegemea Mungu, na uweze kuona matendo halisi ya Mungu—ni hapo tu ndipo mapenzi ya Mungu yatatimizwa. Sasa hivi, watu wengi hawajui jinsi ya kupitia, na wanapokumbana na suala, hawajui jinsi ya kulishughulikia; hawawezi kuipitia kazi ya Mungu, na hawezi kuishi maisha ya kiroho. Lazima uchukue maneno ya Mungu na kuyafanya ndani ya maisha yako ya utendaji.

Wakati mwingine Mungu hukupa aina fulani ya hisia, hisia inayokusababisha upoteze starehe yako ya ndani kabisa, na unapoteza uwepo wa Mungu, kiasi kwamba unatumbukia gizani. Hii ni aina ya usafishaji. Wakati wowote unapofanya kitu chochote, hicho huenda mrama, au kugonga ukuta. Hii ni nidhamu ya Mungu. Wakati mwingine, unapofanya kitu ambacho si cha utiifu na cha uasi kwa Mungu, huenda hakuna mtu mwingine anajua kukihusu—lakini

Mungu anajua. Yeye hatakuachilia, na Atakufundisha nidhamu. Kazi ya Roho Mtakatifu ni yenye kina sana. Kwa makini sana Anatazama kila neno na tendo la watu, kila tendo na mwendo wao, na kila wazo lao na fikira ili watu waweze kupata ufahamu wa ndani wa vitu hivi. Unafanya kitu mara moja na kinaenda mrama, unakifanya kitu tena na bado kinaenda mrama, na hatua kwa hatua utapata kuelewa kazi ya Roho Mtakatifu. Kupitia kufundishwa nidhamu mara nyingi, utajua cha kufanya ili kuwa sambamba na mapenzi ya Mungu na kile kisichoambatana na mapenzi Yake. Mwishowe, utakuwa na majibu sahihi kwa uongozi wa Roho Mtakatifu ndani yako. Wakati mwingine utakuwa muasi na utakemewa na Mungu kutoka ndani. Haya yote hutoka kwa nidhamu ya Mungu. Kama huthamini neno la Mungu, kama unaidharau kazi Yake, Hatashughulika na wewe hata kidogo. Kadiri unavyoyachukulia maneno ya Mungu kwa makini, ndivyo Atakavyokupa nuru zaidi. Sasa hivi, kuna baadhi ya watu katika kanisa ambao wana imani iliyovurugwa na yenye kuchanganyikiwa, na wao hufanya mambo mengi yasiyofaa na kutenda bila nidhamu, na hivyo kazi ya Roho Mtakatifu haiwezi kuonekana wazi ndani yao. Baadhi ya watu huacha nyuma wajibu wao kwa ajili ya kuchuma pesa, kwenda nje kuendesha biashara bila kuwa na nidhamu; mtu wa aina hiyo yuko katika hatari zaidi. Siyo tu kwamba sasa hawana kazi ya Roho Mtakatifu, lakini katika siku zijazo itakuwa vigumu kwa wao kukamilishwa. Kuna watu wengi ambao kwao kazi ya Roho Mtakatifu haiwezi kuonekana na ambao nidhamu ya Mungu haiwezi kuonekana kwao. Wao ni wale ambao hawako wazi juu ya mapenzi ya Mungu na ni wasiojua kazi Yake. Wale ambao wanaweza kusimama imara katikati ya usafishaji, wanaofuata Mungu bila kujali Anachofanya, na angalau wanaweza kusalia, au kutimiza 0.1% ya kile ambacho Petro alitimiza wanafanya vyema, lakini hawana thamani kuhusiana na Mungu kuwatumia. Watu wengi huelewa mambo haraka, wana upendo wa kweli kwa Mungu, na wanaweza kuzidi kiwango cha Petro, na Mungu huwafanyia kazi ya kukamilisha. Nidhamu na nuru huja kwa watu kama hawa, na iwapo kuna jambo ndani yao lisiloambatana na mapenzi ya Mungu, wanaweza kulitupilia mbali mara moja. Watu kama hawa ni dhahabu, fedha na vito—wana thamani ya juu kabisa! Kama Mungu amefanya aina nyingi za kazi lakini bado uko kama mchanga au jiwe, basi huna thamani!

Kazi ya Mungu katika nchi ya joka kubwa jekundu ni ya ajabu na isiyoeleweka. Yeye atalikamilisha kundi moja la watu na kuondoa wengine, kwani kuna kila aina ya watu kanisani—kuna wale wanaopenda ukweli, na wale wasiopenda; kuna wale wanaopitia kazi ya Mungu, na wale wasiopitia; kuna wale wanaofanya wajibu wao, na wale wasiofanya; kuna wale wanaomshuhudia Mungu, na wale wasiomshuhudia—na wengine wao ni wasioamini na watu waovu, na hakika wataondolewa. Kama hujui vizuri kazi ya Mungu, basi utakuwa hasi; hii ni kwa sababu kazi ya Mungu inaweza tu kuonekana katika watu wachache. Wakati huu, itakuwa wazi ni nani ambao wanampenda Mungu kwa kweli na wasiompanda. Wale ambao kweli

wanampenda Mungu wana kazi ya Roho Mtakatifu, huku wale ambao hawampendi kwa kweli watafichuliwa kupitia kila hatua ya kazi Yake. Watakuwa walengwa wa kuondolewa. Watu hawa watafichuliwa katika kipindi cha kazi ya ushindi, na wao ni watu ambao hawana thamani ya kufanywa wakamilifu. Wale ambao wamekamilishwa wamepatwa na Mungu katika ukamilifu wao wote, na wana uwezo wa kumpenda Mungu kama vile alivyokuwa nao Petro. Wale ambao wameshindwa hawana upendo wa hiari, lakini wana upendo usioonyesha hisia, na wao wanalazimika kumpenda Mungu. Upendo wa hiari unakuzwa kwa njia ya uelewa uliopatikana kupitia uzoefu wa vitendo. Upendo huu unachukua moyo wa mtu na unamfanya kujitolea kwa Mungu kwa hiari; maneno ya Mungu yanakuwa msingi wao na wanaweza kuteseka kwa ajili ya Mungu. Bila shaka haya ni mambo yanayomilikiwa na mtu ambaye amekamilishwa na Mungu. Kama unataka tu kushindwa, basi huwezi kuwa na ushuhuda kwa Mungu; kama Mungu angetimiza tu lengo Lake la wokovu kwa njia ya kuwashinda watu, basi hatua ya watenda huduma ingemaliza kazi. Hata hivyo, kuwashinda watu si lengo la mwisho la Mungu, ambalo ni kuwakamilisha watu. Hivyo badala ya kusema kwamba hatua hii ni kazi ni ya kuwashinda watu, sema kuwa ni kazi ya kukamilisha na kuondoa. Baadhi ya watu hawajashindwa kabisa, na katika harakati ya kuwashinda, kundi la watu watafanywa wakamilifu. Vipande hivi viwili vya kazi vinafanywa kwa pamoja. Watu hawajaondoka hata kwa muda mrefu sana kama huu wa kazi, na hili linaonyesha kuwa lengo la ushindi limekuwa na mafanikio—huu ni ukweli wa kushindwa. Usafishaji si kwa ajili ya kushindwa, lakini ni kwa ajili ya kukamilishwa. Bila usafishaji, watu hawangeweza kukamilishwa. Hivyo usafishaji kweli ni wa thamani! Leo kundi moja la watu linakamilishwa na kupatwa. Baraka kumi zilizotajwa hapo awali zote zililengwa kwa wale ambao wamekamilishwa. Kila kitu kuhusu kubadilisha sura zao duniani kunalenga wale ambao wamekamilishwa. Wale ambao hawajakamilishwa hawastahili kupokea ahadi za Mungu.

Ni kwa Kupitia tu Majaribio ya Kuumiza Ndiyo Mnaweza Kujua Kupendeza kwa Mungu

Unampenda Mungu kiasi gani hasa leo? Na unajua kiasi gani hasa kuhusu yote ambayo Mungu amefanya ndani yako? Haya ni mambo unayopaswa kujifunza. Mungu anapowasili duniani, yote ambayo Amefanya ndani ya mwanadamu na kumkubalia mwanadamu kuona ni ili mwanadamu atampenda na kumjua Yeye kweli. Kwamba mwanadamu anaweza kuteseka kwa ajili ya Mungu na ameweza kufikia umbali huu ni, kuhusiana na jambo moja, kwa sababu ya upendo wa Mungu, na kuhusiana na jambo lingine, ni kwa sababu ya wokovu wa Mungu; zaidi ya hayo, ni kwa sababu ya kazi ya hukumu na kuadibu ambayo Mungu ametekeleza ndani ya mwanadamu. Kama hamna hukumu, kuadibu, na majaribio ya Mungu, na kama Mungu hajawafanya mteseke, basi, kusema ukweli, ninyi hammpendi Mungu kweli. Kadiri kazi ya

Mungu ilivyo kuu zaidi ndani ya mwanadamu, na kadri mateso ya mwanadamu yalivyo makuu zaidi, ndivyo inavyoweza kuonyesha zaidi hasa vile kazi ya Mungu ilivyo ya maana, na ndivyo moyo wa mwanadamu unavyoweza kumpenda Mungu kweli zaidi. Unajifunzaje jinsi ya kumpenda Mungu? Bila mateso makali na usafishaji, bila majaribio ya kuumiza—na kama, zaidi ya hayo, yote ambayo Mungu alimpa mwanadamu ingekuwa neema, upendo, na rehema—je, ungeweza kufikia upendo wa kweli kwa Mungu? Kwa upande mmoja, wakati wa majaribio ya Mungu mwanadamu huja kujua kasoro zake, na huona kwamba yeye ni mdogo, wa kudharauliwa, na duni, kwamba hana chochote, na si kitu; kwa upande mwingine, wakati wa majaribio Yake Mungu humuumbia mwanadamu mazingira tofauti yanayomfanya mwanadamu aweze zaidi kupitia kupendeza kwa Mungu. Ingawa maumivu ni makubwa, na wakati mwingine yasiyoshindika—na hata hufikia kiwango cha huzuni ya kuseta—baada ya kuyapitia, mwanadamu huona vile kazi ya Mungu ndani yake ni ya kupendeza, na ni juu ya msingi huu tu ndiyo ndani ya mwanadamu huzaliwa upendo wa kweli kwa Mungu. Leo mwanadamu huona kwamba na neema, upendo na rehema ya Mungu pekee, hana uwezo wa kujijua mwenyewe kweli, sembuse kuweza kujua kiini cha mwanadamu. Ni kupitia tu usafishaji na hukumu ya Mungu, ni wakati tu wa usafishaji kama huo ndiyo mwanadamu anaweza kujua kasoro zake, na kujua kwamba hana chochote. Hivyo, upendo wa mwanadamu kwa Mungu umejengwa juu ya msingi wa usafishaji na hukumu ya Mungu. Kama wewe hufurahia tu neema ya Mungu, na maisha ya familia yenye amani au baraka yakinifu, basi hujampata Mungu, na imani yako kwa Mungu haiwezi kuchukuliwa kama iliyofaulu. Mungu tayari ametekeleza hatua moja ya kazi ya neema katika mwili, na tayari amempa mwanadamu baraka yakinifu—lakini mwanadamu hawezi kufanya mkamilifu na neema, upendo, na rehema pekee. Katika uzoefu wa mwanadamu yeye hukabiliwa na baadhi ya upendo wa Mungu, na huuona upendo na rehema ya Mungu, lakini baada ya kupitia kwa kipindi fulani cha wakati, yeye huona kwamba neema ya Mungu na upendo na rehema Yake hayawezi kumfanya mwanadamu awe mkamilifu, na hayana uwezo wa kufichua kile ambacho ni potovu ndani ya mwanadamu, wala hayawezi kumwondolea mwanadamu tabia yake potovu, au kufanya kuwa kamilifu upendo na imani yake. Kazi ya Mungu ya neema ilikuwa kazi ya kipindi kimoja, na mwanadamu hawezi kutegemea kufurahia neema ya Mungu ili kumjua Mungu.

Ni kupitia nini ndiyo ukamilishaji wa Mungu kwa mwanadamu hutimizwa? Kupitia tabia Yake yenye haki. Tabia ya Mungu hasa huwa na haki, ghadhabu, uadhama, hukumu, na laana, na ukamilishaji Wake wa mwanadamu hasa ni kupitia hukumu. Watu wengine hawaelewi, na huuliza ni kwa nini Mungu anaweza tu kumfanya mwanadamu kuwa mkamilifu kupitia hukumu na laana. Wao husema, “Kama Mungu angemlaani mwanadamu, si mwanadamu angekufa? Kama Mungu angemhukumu mwanadamu, si mwanadamu angelaaniwa? Basi anawezaje hata

hivyo kufanywa mkamilifu?” Hayo ndiyo maneno ya watu wasiojua kazi ya Mungu. Kile ambacho Mungu hulaani ni uasi wa mwanadamu, na kile Anachohukumu ni dhambi za mwanadamu. Ingawa Yeye hunena kwa ukali, na bila kiwango cha hisi hata kidogo, Yeye hufichua yote yaliyo ndani ya mwanadamu, na kupitia maneno haya makali Yeye hufichua kile kilicho muhimu ndani ya mwanadamu, lakini kupitia hukumu kama hiyo, Yeye humpa mwanadamu ufahamu mkubwa wa kiini cha mwili, na hivyo mwanadamu hujitiisha chini ya utii mbele za Mungu. Mwili wa mwanadamu ni wa dhambi, na wa Shetani, ni wa kutotii, na chombo cha kuadibu kwa Mungu—na kwa hiyo, ili kumruhusu mwanadamu kujijua, maneno ya hukumu ya Mungu lazima yamfike na lazima kila aina ya usafishaji itumike; ni wakati huo tu ndiyo kazi ya Mungu inaweza kuwa ya kufaa.

Kutokana na maneno yaliyonenwa na Mungu inaweza kuonekana kwamba tayari Ameulaani mwili wa mwanadamu. Je, haya maneno, basi, ni maneno ya laana? Maneno yaliyonenwa na Mungu hufichua tabia halisi ya mwanadamu, na kupitia ufichuzi kama huo anahukumiwa, na anapona kwamba hawezi kuyaridhisha mapenzi ya Mungu, ndani anahisi huzuni na majuto, anahisi kwamba anapaswa kumshukuru Mungu sana, na asiyetosha kwa ajili mapenzi ya Mungu. Kuna nyakati ambapo Roho wa Mungu hukufundisha nidhamu kutoka ndani, na nidhamu hii hutoka kwa hukumu ya Mungu; kuna nyakati ambapo Mungu hukushutumu na kuuficha uso Wake kutoka kwako, wakati ambapo hakusikilizi, na Hafanyi kazi ndani yako, akikuadibu bila sauti ili kukusafisha. Kazi ya Mungu ndani ya mwanadamu ni hasa ili kuweka wazi tabia Yake yenye haki. Ni ushuhuda gani ambao mwanadamu hatimaye huwa nao kwa Mungu? Yeye hushuhudia kwamba Mungu ni Mungu mwenye haki, kwamba tabia yake ni haki, ghadhabu, kuadibu, na hukumu; mwanadamu hushuhudia kwa tabia yenye haki ya Mungu. Mungu hutumia hukumu Yake kumfanya mwanadamu awe mkamilifu, Amekuwa Akimpenda mwanadamu, na kumwokoia mwanadamu—lakini ni kiasi gani kiko ndani ya upendo Wake? Kuna hukumu, uadhama, ghadhabu, na laana. Ingawa Mungu alimlaani mwanadamu katika wakati uliopita, Hakumtupa mwanadamu kabisa ndani ya shimo la kuzimu, lakini Alitumia njia hiyo kuisafisha imani ya mwanadamu; Hakumuua mwanadamu, lakini alitenda ili kumfanya mwanadamu awe mkamilifu. Kiini cha mwili ni kile ambacho ni cha Shetani—Mungu alikisema sahihi kabisa—lakini ukweli unaotekelezwa na Mungu haukamilishwi kufuatana na maneno Yake. Yeye hukulaani ili uweze kumpenda, na ili uweze kujua kiini cha mwili; Yeye hukuadibu ili uweze kuamshwa, kukuruhusu wewe ujue kasoro zilizo ndani yako, na kujua kutostahili kabisa kwa mwanadamu. Hivyo, laana za Mungu, hukumu Yake, na uadhama na ghadhabu Yake—yote ni kwa ajili ya kumfanya mwanadamu awe mkamilifu. Yote ambayo Mungu anafanya leo, na tabia yenye haki ambayo Yeye huifanya kuwa wazi ndani yenu—yote ni kwa ajili ya kumfanya mwanadamu awe mkamilifu, na huo ndio upendo wa Mungu.

Katika dhana za mwanadamu za kitamaduni, upendo wa Mungu ni neema Yake, fadhili, na huruma kwa udhaifu wa mwanadamu. Ingawa mambo haya pia ni upendo wa Mungu, yanaegemea upande mmoja sana, na si njia za msingi ambazo kwazo Mungu humfanya mwanadamu kuwa mkamilifu. Wakati ambapo watu wengine wameanza tu kumwamini Mungu, ni kwa sababu ya ugonjwa. Ugonjwa huu ni neema ya Mungu kwako; bila huo, hungemwamini Mungu, na kama hungemwamini Mungu basi hungefika umbali huu—na hivyo hata neema hii ni upendo wa Mungu. Katika wakati wa kumwamini Yesu, watu walifanya mengi ambayo hayakupendwa na Mungu kwa sababu hawakuelewa ukweli, lakini Mungu ana upendo na rehema, na Amemleta mwanadamu umbali huu, na ingawa mwanadamu haelewi chochote, bado Mungu humruhusu mwanadamu amfuate Yeye, na, zaidi ya hayo, Amemwongoza mwanadamu mpaka leo. Je, huu si upendo wa Mungu? Kile ambacho kinadhihirishwa katika tabia ya Mungu ni upendo wa Mungu—hili ni sahihi bila shaka! Wakati ambapo ujenzi wa kanisa ulifikia kilele chake, Mungu alifanya hatua ya kazi ya watendaji huduma na akamtupa mwanadamu katika shimo la kuzimu. Maneno ya wakati wa watendaji huduma yote yalikuwa laana: laana za mwili wako, laana za tabia yako potovu ya kishetani, na laana za mambo kukuhusu wewe ambayo hayayaridhishi mapenzi ya Mungu. Kazi iliyofanywa na Mungu katika hatua hiyo ilidhihirishwa kama uadhama, karibukaribu sana baadaye Mungu alitekeleza hatua ya kazi ya kuadibu, na kisha kukaja majaribio ya kifo. Katika kazi kama hiyo, mwanadamu aliona ghadhabu, uadhama, hukumu, na kuadibu kwa Mungu, lakini aliona pia neema ya Mungu, na upendo na rehema Yake; yote aliyofanya Mungu, na yote yaliyodhihirishwa kama tabia Yake, ulikuwa upendo wa mwanadamu, na yote ambayo Mungu alifanya yaliweza kutimiza mahitaji ya mwanadamu. Aliyafanya ili kumfanya mwanadamu awe mkamilifu, na Alimkimu mwanadamu kadri ya kimo chake. Kama Mungu hangefanya hili, mwanadamu hangekuwa na uwezo wa kuja mbele za Mungu, na hangekuwa na njia ya kuujua uso wa kweli wa Mungu. Tangu wakati ambapo mwanadamu alianza kwa mara ya kwanza kumwamini Mungu mpaka leo, Mungu amemkimu mwanadamu polepole kwa mujibu wa kimo chake, ili kwamba, ndani, mwanadamu amekuja kumjua Yeye polepole. Ni kwa kuweza kufika leo tu ndiyo mwanadamu ametambua hasa vile hukumu ya Mungu ni ya ajabu. Hatua ya kazi ya watendaji huduma ilikuwa tokeo la kwanza la kazi ya laana tangu wakati wa uumbaji mpaka leo. Mwanadamu alilaaniwa kwenda katika shimo la kuzimu. Kama Mungu hangefanya hivyo, leo mwanadamu hangekuwa na ufahamu wa kweli wa Mungu; ilikuwa kupitia tu laana ya Mungu ndiyo mwanadamu alikutana rasmi na tabia ya Yake. Mwanadamu alifichuliwa kupitia majaribu ya watendaji huduma. Aliona kwamba uaminifu wake haukukubalika, kwamba kimo chake kilikuwa kidogo sana, kwamba hakuwa na uwezo wa kuridhisha mapenzi ya Mungu, na kwamba madai yake ya kumridhisha Mungu wakati wote yalikuwa maneno matupu tu. Ingawa katika hatua ya kazi ya watendaji huduma Mungu alimlaani mwanadamu, tukitazama nyuma leo, hatua hiyo ya kazi ya Mungu ilikuwa ya ajabu:

Ilileta mgeuzo mkubwa kwa mwanadamu, na kusababisha mabadiliko makuu katika tabia yake ya maisha. Kabla ya wakati wa watendaji huduma, mwanadamu hakuelewa chochote kuhusu ukimbizaji wa maisha, ni nini maana ya kumwamini Mungu, au hekima ya kazi ya Mungu, wala hakufahamu kwamba kazi ya Mungu inaweza kumjaribu mwanadamu. Tangu wakati wa watendaji huduma mpaka leo, mwanadamu huona vile kazi ya Mungu ni ya ajabu, haiwezi kueleweka kwa mwanadamu, na akitumia akili yake hawezi kufikiria jinsi Mungu hufanya kazi, na pia huona vile kimo chake ni kidogo na kwamba kiasi kikubwa chake ni cha kutotii. Mungu alipomlaani mwanadamu, ilikuwa ili Atimize athari, na Hakumuua mwanadamu. Ingawa Alimlaani mwanadamu, Alifanya hivyo kupitia maneno, na laana Zake hazikumwangukia mwanadamu kwa kweli, kwani kile ambacho Mungu alilaani kilikuwa kutotii kwa mwanadamu, na kwa hiyo maneno ya laana Zake pia yalikuwa kwa ajili ya kumfanya mwanadamu awe mkamilifu. Kama Mungu atamhukumu mwanadamu au kumlaani, yote mawili humfanya mwanadamu kuwa mkamilifu: Yote mawili yanafanywa ili kukifanya kamili kile ambacho ni kichafu ndani ya mwanadamu. Kupitia njia hii mwanadamu anasafishwa, na kile ambacho kinakosekana ndani ya mwanadamu kinafanywa kamilifu kupitia maneno na kazi Yake. Kila hatua ya kazi ya Mungu—kama ni maneno makali, au hukumu, au kuadibu—humfanya mwanadamu kuwa mkamilifu, na inafaa kwa uhalisi. Kote kote katika enzi zote Mungu hajawahi kufanya kazi kama hii; leo, Yeye hufanya kazi ndani yenu ili muweze kufahamu hekima Yake. Ingawa mmepitia maumivu fulani ndani yenu, mioyo yenu inajisikia thabiti na kwa amani; ni baraka yenu kuweza kufurahia hatua hii ya kazi ya Mungu. Haijalishi kile mnachoweza kupata katika siku za baadaye, yote mnayoona kuhusu kazi ya Mungu ndani yenu leo ni upendo. Kama mwanadamu hapitii hukumu na kuadibu kwa Mungu, matendo yake na ari daima yatakuwa nje, na tabia yake daima itaendelea kutobadilika. Je, hii inahesabika kama kupatwa na Mungu? Leo, ingawa bado kuna mengi ndani ya mwanadamu ambayo ni yenye kiburi na yenye majivuno, tabia ya mwanadamu ni imara zaidi kuliko awali. Mungu kukushughulikia wewe ni ili kukuokoa, na ingawa unaweza kuhisi maumivu kidogo wakati huo, siku itafika ambapo kutatokea mabadiliko katika tabia yako. Wakati huo, utakumbuka ya nyuma na kuona vile kazi ya Mungu ni ya hekima, na huo utakuwa wakati ambao utaweza kufahamu kwa kweli mapenzi ya Mungu. Leo, kuna watu wengine ambao husema kwamba wanafahamu mapenzi ya Mungu—lakini hiyo si ya kweli kamwe, wao wanazungumza upuuzi, kwa sababu wakati huu bado hawajafahamu kama mapenzi ya Mungu ni kumwokoza mwanadamu au kumlaani mwanadamu. Labda huwezi kuliona kwa dhahiri sasa, lakini siku itafika ambapo utaona kwamba siku ya kutukuzwa kwa Mungu imefika, na uone jinsi ni ya maana kumpenda Mungu, ili utakuja kuyajua maisha ya binadamu, na mwili wako utaishi katika ulimwengu wa kumpenda Mungu, kwamba roho yako itawekwa huru, maisha yako yatajaa furaha, na kwamba daima utakuwa karibu na Mungu, na utamtegemea Mungu daima. Wakati huo, utajua kweli jinsi kazi ya Mungu ni ya thamani leo.

Leo, watu wengi sana hawana ufahamu huo. Wao huamini kwamba mateso hayana thamani, wao hukanwa na ulimwengu, maisha yao ya nyumbani yamesumbuliwa, wao si wapendwa wa Mungu, na matazamio yao ni matupu. Kuteseka kwa watu wengine hufikia kiwango fulani, na fikira zao hugeukia kifo. Huu si upendo wa kweli kwa Mungu; watu kama hao ni waoga, hawana ustahamilivu, wao ni wadhaifu na wasio na nguvu! Mungu ana hamu ya mwanadamu kumpenda Yeye, lakini kadri mwanadamu anavyompenda Yeye, ndivyo kuteseka kwa mwanadamu huwa kwingi zaidi, na kadri mwanadamu anavyompenda Yeye, ndivyo majaribio ya mwanadamu huwa makubwa zaidi. Ikiwa unampenda Yeye, basi kila aina ya mateso yatakufika—na ikiwa humpendi, basi labda kila kitu kitaendelea kwa urahisi kwako, na kila kitu kinachokuzunguka kitakuwa kitulivu kwako. Unapompenda Mungu, utahisi kwamba mengi kandokando yako hayawezi kushindikana, na kwa sababu kimo chako ni kidogo sana utasafishwa; aidha, huwezi kumridhisha Mungu, na daima utahisi kwamba mapenzi ya Mungu ni ya juu sana, kwamba hayawezi kufikiwa na mwanadamu. Kwa sababu ya haya yote utasafishwa—kwa sababu kuna udhaifu mwingi ndani yako, na mengi yasiyoweza kuridhisha mapenzi ya Mungu, utasafishwa ndani. Lakini lazima muone kwa dhahiri kwamba utakaso hutimizwa tu kupitia usafishaji. Hivyo, katika siku hizi za mwisho lazima muwe na ushuhuda kwa Mungu. Haijalishi mateso yenu ni makubwa vipi, mnapaswa kuendelea hadi mwisho kabisa, na hata wakati wa pumzi yenu ya mwisho, bado lazima muwe waaminifu kwa Mungu, na kudhibitiwa na Mungu; huku pekee ndiko kumpenda Mungu kweli, na huu pekee ndio ushuhuda thabiti na mkubwa sana. Unapojaribiwa na Shetani, unapaswa kusema: “Moyo wangu ni wa Mungu, na Mungu tayari amenipata. Siwezi kukuridhisha wewe—lazima nitoe kila kitu changu ili kumridhisha Mungu.” Kadri unavyomridhisha Mungu, ndivyo Mungu hukubariki zaidi, na ndivyo nguvu za upendo wako kwa Mungu huwa kuu zaidi; kwa hiyo, vilevile, utakuwa na imani na azimio, na utahisi kwamba hakuna kilicho na thamani zaidi au cha maana kuliko kutumia maisha ukimpenda Mungu. Inaweza kusemwa kwamba mwanadamu anatakiwa tu kumpenda Mungu ili kuishi bila huzuni. Ingawa kuna nyakati ambazo mwili wako ni dhaifu na unazongwa na matatizo mengi ya kweli, katika nyakati hizi utamtegemea Mungu kweli, na ndani ya roho yako utafarijiwa, na utahisi hakika, na kwamba una kitu cha kutegemea. Kwa njia hii, utaweza kushinda hali nyingi, na kwa hiyo hutalalamika kuhusu Mungu kwa sababu ya uchungu unaopitia; utataka kuimba, kucheza, na kuomba, kukusanyika na kuwasiliana kwa karibu, kumfikiria Mungu, na utahisi kwamba watu wote, mambo, na vitu vilivyo kandokando yako ambavyo vimepangwa na Mungu vinafaa. Kama humpendi Mungu, yote ambayo unategemea yatakuwa yenye kero kwako, hakuna kitakachokuwa cha kufurahisha machoni mwako; ndani ya roho yako hutakuwa huru bali wa kudhulumiwa, moyo wako daima utalalamika kuhusu Mungu, na daima utahisi kwamba unapitia mateso mengi sana, na kwamba ni udhalimu sana. Kama hufuatilii kwa ajili ya furaha, bali ili umridhishe Mungu na kutoshtakiwa na Shetani, basi ukimbizaji kama huo utakupa nguvu nyingi

za kumpenda Mungu. Mwanadamu anaweza kutekeleza yote yanayonenwa na Mungu, na yote ayafanyayo yanaweza kumridhisha Mungu—hii ndiyo maana ya kuwa na hakika. Kufuatilia ridhaa ya Mungu ni kuutumia upendo wa Mungu kutia maneno Yake katika vitendo; pasipo kutia maanani wakati—hata kama wengine hawana nguvu—ndani yako bado kuna moyo unaompenda Mungu, ambao unamtamani Mungu sana, na humkosa Mungu. Hiki ni kimo halisi. Jinsi ambavyo kimo chako ni kikubwa hasa hutegemea jinsi upendo wako kwa Mungu ulivyo mkuu, kama unaweza kusimama imara wakati unajaribiwa, kama wewe ni mdhaifu hali fulani inapokujia, na kama unaweza kusimama imara wakati ambapo ndugu zako wanakukataa; majilio ya ukweli yataonyesha hasa upendo wako kwa Mungu ukoje. Inaweza kuonekana kutoka kwa kazi nyingi ya Mungu kwamba Mungu kweli anampenda mwanadamu, ni hasa tu macho ya roho ya mwanadamu bado hayajafunguliwa kabisa, na hawezi kufahamu kazi nyingi ya Mungu, na mapenzi ya Mungu, na vitu vingi ambavyo ni vya kupendeza kuhusu Mungu; mwanadamu ana upendo kidogo sana wa kweli kwa Mungu. Umemwamini Mungu katika wakati huu wote, na leo Mungu amezuia njia zote za kutoroka. Kusema kwa kweli, huna chaguo lingine ila kuifuata njia sahihi, njia sahihi ambayo umeelekezwa kwayo kwa hukumu kali na wokovu mkubwa kabisa wa Mungu. Ni baada tu ya kupitia taabu na usafishaji ndiyo mwanadamu hujua kwamba Mungu ni wa kupendeza. Baada ya kupitia mpaka leo, inaweza kusemwa kwamba mwanadamu amekuja kujua sehemu ya kupendeza kwa Mungu—lakini hili bado halitoshi, kwa sababu mwanadamu amepungukiwa sana. Lazima apate uzoefu zaidi wa kazi ya Mungu ya ajabu, na zaidi ya usafishaji wote wa mateso uliowekwa na Mungu. Ni wakati huo tu ndiyo tabia ya maisha ya mwanadamu itaweza kubadilishwa.

Kumpenda Mungu tu Ndiko Kumwamini Mungu Kweli

Mnapotaka kumpenda na kumjua Mungu leo, kwa upande mmoja ni lazima mstahimili mateso, usafishaji, na kwa ule upande mwingine, ni lazima mgharamike. Hakuna funzo lililo kubwa kuliko lile la kumpenda Mungu, na inaweza kusemwa kuwa funzo ambalo watu hujifunza katika maisha yao yote ya imani ni jinsi ya kumpenda Mungu. Hii ni kusema, kama unamwamini Mungu ni lazima umpende Mungu. Ikiwa unamwamini tu Mungu lakini humpendi, hujapata ufahamu wa Mungu, na hujawahi kumpenda Mungu kwa upendo wa kweli utokao moyoni mwako, basi imani yako kwa Mungu ni bure; kama katika imani yako kwa Mungu humpendi Mungu, basi unaishi bure, na maisha yako yote ndiyo ya duni zaidi kwa maisha yote. Ikiwa katika maisha yako yote hujawahi kumpenda au kumtosheleza Mungu, basi kuna haja gani ya kuishi? Kuna haja gani ya imani yako kwa Mungu? Huku si kuharibu nguvu? Hii ni kusema, kama watu wanataka kuamini na kumpenda Mungu, ni sharti wagharamike. Badala ya kujaribu kuenenda kwa namna fulani kwa nje tu, wanapaswa watafute utambuzi wa kweli kutoka ndani ya mioyo yao. Ikiwa unapenda sana kuimba na kucheza lakini huwezi kuonyesha ukweli katika

vitendo, unaweza kusemekana kwamba unampenda Mungu? Kumpenda Mungu kunahitaji utafutaji wa mapenzi ya Mungu katika mambo yote, na kwamba ujisaili wewe mwenyewe kwa kina jambo lolote likikutokea, kujaribu kujua mapenzi ya Mungu na kujaribu kuona mapenzi ya Mungu ni yapi katika suala hili, Anataka ufanikishe nini, na ni jinsi gani utayajali mapenzi Yake? Kwa mfano: jambo fulani linafanyika linalokutaka uvumilie hali ngumu, wakati huo unapaswa ufahamu ni nini mapenzi ya Mungu, na ni jinsi gani unapaswa kuyajali mapenzi ya Mungu. Usijiridhishe mwenyewe: Jiweke kando kwanza. Hakuna kitu kilicho duni kuliko mwili. Ni lazima udhamirie kumridhisha Mungu, na ni lazima utekeleze wajibu wako. Katika mawazo kama hayo, Mungu atakupua nuru ya kipekee katika jambo hili, na moyo wako pia utapata faraja. Jambo lolote likikutendelea, liwe dogo au kubwa, ni sharti kwanza ujiweke pembeni na kuuona mwili kama kitu duni zaidi kuliko vitu vyote. Kadiri unavyouridhisha mwili zaidi, ndivyo unavyochukua uhuru zaidi; ukiuridhisha mara hii, wakati mwingine utataka zaidi. Hili linapoendelea, watu wanapata kuupenda mwili hata zaidi. Mwili mara zote una tamaa kupita kiasi, mara zote mwili unakutaka uuridhishe, na kwamba uutoshesheleze kwa ndani, iwe ni katika chakula unachokula, unachokivaa, au kuwa na hasira katika matendo yako, au kuushawishi udhaifu na uzembe wako... Kadiri unavyouridhisha mwili zaidi, ndivyo tamaa yake inaongezeka, na jinsi mwili unavyopotoka zaidi, hadi kufikia kiwango ambacho miili ya watu inahodhi dhana nzito, na kutomtii Mungu, na kujiinua, na kuanza kuishuku kazi ya Mungu. Kadiri unavyouridhisha mwili zaidi, ndivyo udhaifu wa mwili unavyokuwa mkubwa; daima utahisi kuwa hakuna anayekuonea huruma kwa udhaifu wako, daima utaamini kuwa Mungu amezidi sana, na utasema: Mungu anawezaje kuwa mkali namna hii? Ni kwa nini Hawezi kuwapa watu nafasi? Watu wakiudekeza sana mwili, na kuupenda kupindukia, basi wanajiangamiza wao wenyewe. Ikiwa unampenda Mungu kwa dhati, na hauridhishi mwili, basi utaona kuwa kila anachokifanya Mungu ni chenye haki sana, na kizuri sana, na kwamba laana Yake kwa uasi wako na hukumu ya udhalimu wako ni haki. Zitakuwepo nyakati ambapo Mungu atakurudi na kukufundisha nidhamu, na kuanzisha mazingira ya kukukasirisha, na kukushurutisha uje mbele Zake—na daima utahisi kuwa anachokifanya Mungu ni cha ajabu. Hivyo utahisi kana kwamba hakuna uchungu mwingi, na kwamba Mungu anapendeza. Ukifuata udhaifu wa mwili, na kusema kwamba Mungu amezidi, basi daima utahisi uchungu na daima utahuzunika, na utakosa uwazi kuhusu kazi yote ya Mungu na itaonekana kana kwamba Mungu hana huruma kwa udhaifu wa mwanadamu, na Hatambui shida za mwanadamu. Hivyo utajihisi mnyonge na mpweke, kana kwamba umekumbwa na dhuluma kubwa, na wakati huo utaanza kulalama. Kadiri unavyoutoshesheleza udhaifu wa mwili, ndivyo unavyohisi kuwa Mungu anazidi, hadi inakuwa mbaya kiasi kwamba unaikana kazi ya Mungu, na kuanza kumpinga Mungu na kujaa uasi. Hivyo unafaa kuuasi mwili na usiutosheleze: “Mume wangu(mke), watoto, matarajio, ndoa, familia—hakuna hata moja kati ya haya ambalo ni la thamani! Moyoni mwangu mna

Mungu pekee na nitajaribu kumridhisha Mungu kadiri ya uwezo wangu, na si kuuridhisha mwili.” Lazima uwe na azimio hili. Daima ukiwa na azimio hili, basi ukiuweka ukweli katika vitendo, na kujiweka kando, utaweza kufanya hivyo kwa juhudi kidogo. Inasemekana kuwa kulikuwepo na mkulima aliyeona nyoka barabarani aliyekuwa ameganda. Huyu mkulima alimchukua yule nyoka na kumweka kifuani mwake, na baada ya yule nyoka kuamka alimuuma yule mkulima hadi akafa. Miili ya wanadamu ni kama yule nyoka: asili yake ni kuyadhuru maisha yao—na ikipata mbinu yake kikamilifu, maisha yako yanapotea. Mwili ni wa Shetani. Kuna tamaa kupita kiasi ndani yake, hujithamini wenyewe, unafurahia faraja, na kushangilia burudani, kujiachilia katika uvivu na uzembe, na baada ya kuuridhisha kwa kiwango fulani mwishowe utakuangamiza. Hivi ni kusema, ukiuridhisha sasa, wakati mwingine utakuomba zaidi. Daima mwili una tamaa na matakwa kupita kiasi, na unajinufaisha kutokana na wewe kuutosheleza mwili na kukufanya uufurahie hata zaidi na kuishi katika starehe zake—na ikiwa hutaushinda, mwishowe utajiangamiza mwenyewe. Iwapo utapata uzima mbele za Mungu, na namna hatima yako itakavyokuwa, inategemea uasi wako dhidi ya mwili utakuwa wa namna gani. Mungu amekuokoa, na kukuteua na kukuamulia kabla, bado ikiwa leo hauko radhi kumridhisha, hauko radhi kuuweka ukweli katika vitendo, hauko radhi kuuasi mwili wako kwa moyo umpendao Mungu kwa dhati, hatimaye utajiangamiza mwenyewe, na kwa hivyo utapitia mateso mengi. Ikiwa mara zote unautosheleza mwili, Shetani atakumeza hatua kwa hatua, na kukuacha bila uzima, au upako wa Roho, hadi siku itafika ambayo ndani utakuwa giza. Ukiishi katika giza, utakuwa umetekwa nyara na Shetani, hutakuwa na Mungu tena moyoni mwako, na wakati ule utaukataa uwepo wa Mungu na kumwacha. Kwa hivyo, ikiwa watu wanataka kumpenda Mungu, ni lazima walipe gharama ya uchungu na kupitia shida. Hakuna haja ya hamasa za nje na shida, kusoma zaidi na kuzungukazunguka zaidi; badala yake, wanafaa kuweka kando vitu vilivyomo ndani yao: mawazo kupita kiasi, maslahi ya kibinafsi, na masuala yao binafsi, fikira, na nia. Hayo ndiyo mapenzi ya Mungu.

Ushughulikiaji wa Mungu juu ya tabia za nje za watu ni sehemu moja ya kazi Yake; kwa mfano, kushughulikia ubinadamu wa watu wa nje, usiokuwa wa kawaida, au maisha na tabia zao, njia na desturi zao, na vilevile vitendo vyao vya nje, na hamasa zao. Lakini Anapowataka watu wauweke ukweli katika vitendo na wabadilishe tabia zao, kimsingi kinachoshughulikiwa hapa ni motisha na mawazo yaliyo ndani yao. Kushughulikia tabia zako za nje tu si kugumu; ni sawa na kukukataza kula vitu uvipendavyo, jambo ambalo ni rahisi. Kinachogusia fikira zilizo ndani yako, hata hivyo, si rahisi kukiachia. Inawahitaji wauasi mwili wao, na kulipa gharama, na kuteseka mbele za Mungu. Hii ndiyo hali hasa katika nia za watu. Tangu watu waanze kumwamini Mungu, wamekuwa na nia ambazo si sahihi. Wakati ambapo huweki ukweli katika vitendo, unahisi kuwa motisha zako ni sahihi, lakini jambo likikutokea, utaona kuwa kuna

motisha nyingi ndani zisizo sahihi. Hivyo, Mungu akiwafanya watu kuwa wakamilifu, Anawafanya kugundua kuwa kuna dhana nyingi ndani yao ambazo zinawazuia kumfahamu Mungu. Ukitambua kuwa motisha zako zina makosa, kama unaweza kuacha kutenda kulingana na motisha na dhana zako, na unaweza kuwa na ushuhuda wa Mungu na kusimama imara katika msimamo wako kwa kila lifanyikalo kwako, hili linathibitisha kuwa umeuasi mwili wako. Ukiasi dhidi ya mwili wako, bila shaka kutakuwa na vita ndani yako. Shetani atajaribu kufanya watu kuifuata, atajaribu kuwafanya wafuate dhana za kimwili na kutekeleza maslahi ya kimwili—ila maneno ya Mungu yatawapa nuru watu na kuwaangazia kwa ndani, na wakati huu itakuwa juu yako ikiwa utamfuata Mungu au utamfuata Shetani. Mungu anawataka watu kuweka ukweli katika matendo kimsingi kushughulikia mambo yaliyo ndani yao, kushughulikiwa fikira zao, na dhana zao ambazo haziufuati moyo wa Mungu. Roho Mtakatifu huwagusa watu ndani ya mioyo yao, na kuwapa nuru na mwangaza. Kwa hivyo katika tukio lolote katika vita: Kila wakati watu wanapoweka ukweli katika vitendo, au kuweka mapenzi ya Mungu katika vitendo, huwa kuna vita vikali, na japokuwa mambo yanaweza kuonekana shwari katika miili yao, ila ndani ya mioyo yao kutakuwa na vita vya kufa na kupona—na ni baada tu ya hivi vita vikali, baada ya kutafakari kwa kina, ndipo ushindi au kushindwa kunaweza kuamuliwa. Mtu anashindwa kujua ama acheke au alie. Kwa sababu motisha nyingi ndani ya watu zina makosa, ama kwa sababu kazi kubwa ya Mungu inakinzana na dhana zao, watu wakiuweka ukweli katika vitendo vita vikali huzuka kisirisiri. Baada ya kuuweka huu ukweli katika vitendo, kisirisiri watu watakuwa wamemwaga machozi mengi sana ya huzuni kabla ya kuamua kumridhisha Mungu. Ni kwa sababu ya vita hivi watu huvumilia shida na usafishaji; huku ni kuteseka kwa kweli. Vita vikikukabili, kama unaweza kusimama kweli upande wa Mungu, utaweza kumridhisha Mungu. Katika harakati ya kutenda ukweli, hakupekiki kwamba mtu atateseka kwa ndani; ikiwa, wanapoweka ukweli katika vitendo, kila kitu ndani yao kingekuwa sawa, basi wasingehitaji kufanywa wakamilifu na Mungu, na kusingekuwa na vita, na hawangeteseka. Ni kwa sababu kuna mambo mengi ndani ya watu ndipo hawafai kutumiwa na Mungu, na tabia nyingi za uasi wa mwili, ndipo watu wanapaswa kujifunza funzo la kuasi dhidi ya mwili kwa kina zaidi. Huku ndiko Mungu anaita kuteseka ambako Alimtaka mwanadamu kushiriki Naye. Ukikumbana na shida, fanya hima na umwombe Mungu: Ee Mungu! Ninataka kukuridhisha, ninataka kustahimili mateso ya mwisho ili kuuridhisha moyo Wako, na bila kujali kuwa vikwazo ninavyokumbana navyo ni vikubwa kiasi gani, bado ni sharti nikuridhishe. Hata ikiwa ni kuyatoa maisha yangu yote, bado ni sharti nikuridhishe! Ukiomba na hili azimio utaweza kusimama imara katika ushuhuda wako. Kila wawekapo ukweli katika vitendo, kila wapitiapo usafishaji, kila wanapojaribiwa, na kila wakati kazi ya Mungu inapowashukia, watu wanapitia mateso makubwa. Haya yote ni mtihani wa watu, na kwa hivyo ndani yao wote mna vita. Hii ndiyo gharama hasa wanayolipa. Kusoma zaidi neno la Mungu na kuzungukazunguka zaidi, kwa

namna fulani ni gharama. Ndiyo watu wanapaswa kufanya, ndio wajibu wao, na jukumu ambalo ni sharti walitimize, lakini ni lazima watu waweke kando yale yanayofaa kuwekwa kando. Ikiwa hamwezi, basi haijalishi mateso yako yatakuwa makubwa kiasi gani, na utazunguka kiasi gani, yote yatakuwa bure! Hivi ni kusema, ni mabadiliko ndani yako tu yanaweza kuamua iwapo mateso yako ya nje yana thamani. Tabia yako ya ndani ikibadilika na ikiwa umeweka ukweli katika vitendo, basi mateso yako yote ya nje yatapata kibali cha Mungu; ikiwa hakujakuwa na mabadiliko katika tabia yako ya ndani, basi haijalishi unateseka kiasi gani au unazungukazunguka kiasi gani nje, hakutakuwa na kibali kutoka kwa Mungu—na mateso ambayo hayajaidhinishwa na Mungu ni bure! Hivyo, kama gharama ambayo umelipa imedhinishwa na Mungu inaamuliwa na kama umekuwa na mabadiliko ndani yako au la, na kama unatia ukweli katika vitendo na kuasi dhidi ya motisha na dhana zako mwenyewe ili kupata ridhaa ya mapenzi ya Mungu, ufahamu wa Mungu, na uaminifu kwa Mungu. Haijalishi unazungukazunguka kiasi gani, ikiwa hujawahi kujua kuasi dhidi ya motisha zako, unatafuta tu matendo na hamasa za nje, na usitilie maanani maisha yako, basi taabu zako zitakuwa zimepita bure. Ikiwa una kitu unachotaka kusema katika mazingira fulani, ila kwa ndani unahisi kwamba kukisema si sawa, kwamba kukisema hakuna faida kwa ndugu na dada zako, na kinaweza kuwadhuru, basi na usikiseme, uchague kuumia kwa ndani, kwa kuwa haya maneno hayawezi kuridhisha mapenzi ya Mungu. Wakati huu, kutakuwa na vita ndani yako, lakini utakuwa tayari kuumia na kuviacha uvipendavyo, utakuwa radhi kustahimili haya mateso ili kumridhisha Mungu na ingawa utaumia kwa ndani, hutautosheleza mwili, na moyo wa Mungu utakuwa umeridhishwa, hivyo utafarijika kwa ndani. Kwa hakika huku ni kulipa gharama, na ndiyo gharama inayotakiwa na Mungu. Ukitenda kwa njia hii, kwa hakika Mungu atakubariki; ikiwa huwezi kulifanikisha hili, basi haijalishi unaelewa kiasi gani, au unaweza kunena vyema kiasi gani, yote haya hayatafaa kitu! Katika njia ya kumpenda Mungu, ikiwa unaweza kusimama upande wa Mungu anapopigana na Shetani, na usimgeukie Shetani, basi utakuwa umefanikisha mapenzi ya Mungu, na utakuwa umesimama imara katika ushuhuda wako.

Katika kila hatua ya kazi anayoifanya Mungu ndani ya watu, kwa nje inaonekana kama maingiliano kati ya watu, kana kwamba yalizaliwa kwa mipango ya wanadamu au kutokana na kuingilia kwa wanadamu. Ila kisirisiri, hatua ya kazi, na kila kitu kinachotendeka, ni pingamizi la Shetani kwa Mungu, na huhitaji watu kuwa imara katika ushuhuda wao kwa Mungu. Kwa mfano, tazama wakati Ayubu alijaribiwa: kisirisiri, Shetani alikuwa akiwekeana dau na Mungu, na kilichomtokea Ayubu kilikuwa ni matendo ya wanadamu, na kuingilia kwa wanadamu. Kuna pingamizi la Shetani kwa Mungu katika kila hatua ambayo Mungu anatenda ndani yenu—katika kila kitu kuna vita. Kwa mfano, ikiwa unawabagua ndugu na dada zako, utakuwa na maneno ambayo unataka kusema—maneno unayohisi huenda yasimpendeze Mungu—lakini

usipoyasema, utahisi kutoridhika ndani, na kwa wakati huu vita vitazuka ndani yako: “Niseme au nisiseme?” Hivi ndivyo vita. Kwa hivyo, katika kila jambo unalopitia kuna vita, na wakati kuna vita ndani yako, kutokana na ushirikiano wako na kuteseka kwako, Mungu anafanya kazi ndani yako. Hatimaye unaweza kuliweka kando jambo lenyewe na ghadhabu yako inazimika. Hiyo ndiyo athari ya ushirika wako na Mungu. Kila kitu wafanyacho watu kinawahitaji kulipa gharama fulani katika juhudi zao. Bila taabu ya kweli, hawawezi kumridhisha Mungu, hata hawakaribii kumridhisha Mungu, na wanarusha tu maneno matupu! Je, haya maneno matupu yaweza kumridhisha Mungu? Wakati Mungu na Shetani wanapigana katika milki ya kiroho, utamridhishaje Mungu, na utasimamaje imara katika ushuhuda wako Kwake? Unapaswa kujua kuwa kila kitu unachokipitia ni majaribu makubwa na ndipo Mungu hukuhitaji kuwa na ushuhuda. Kwa nje yataonekana kama mambo madogo; lakini haya mambo yakitendeka huonyesha kama unampenda Mungu au la. Ikiwa unampenda, utaweza kusimama imara katika ushuhuda wako Kwake, na ikiwa hujaweka upendo Wake katika vitendo, hili linaonyesha kuwa wewe si Mtu ambaye anapenda kuuweka ukweli katika vitendo, kwamba huna ukweli, huna uzima, kuwa wewe ni makapi! Mambo huwatokea watu wakati Mungu anawataka wasimame imara katika ushuhuda wao Kwake. Hakuna kubwa lililokutendekeza kwa sasa, na huna ushuhuda mkubwa, lakini kila chembe ya maisha yako ya kila siku inahusiana na ushuhuda kwa Mungu. Ikiwa utawavutia ndugu na dada zako, wanafamilia, na kila aliye karibu nawe; ikiwa siku moja wasioamini watakuja na wavutiwe na yote unenayo na utendayo, na kuona kuwa yote afanyayo Mungu ni ya ajabu, basi utakuwa umekuwa na ushuhuda. Ijapokuwa huna ufahamu na wewe si mwerevu sasa, kupitia kwa kufanywa mkamilifu na Mungu, unaweza kumridhisha na kuzingatia mapenzi Yake, ukiwaoshyesha wengine kazi kubwa Aliyofanya miongoni mwa watu wenye ubora duni wa tabia. Watu wanapokuja kumjua Mungu na kuwa washindi mbele ya Shetani, waaminifu kwa Mungu kwa kiwango kikubwa, basi hakuna aliye na uthabiti kuliko hili kundi la watu, na huu ndio ushuhuda mkubwa zaidi. Ijapokuwa huwezi kufanya kazi kubwa, unaweza kumridhisha Mungu. Wengine hawawezi kuyaacha mawazo yao, ila wewe unaweza; wengine hawawezi kuwa na ushuhuda kwa Mungu wakati wa mapito yao ya kweli, ila unaweza kutumia hadhi na matendo yako ya kweli kulipia mapenzi ya Mungu na kuwa na ushuhuda mkubwa Kwake. Hili ndilo huhesabika kama mapenzi ya kweli kwa Mungu. Ikiwa huliwezi hili, basi hutoi ushuhuda miongoni mwa jamaa zako, miongoni mwa ndugu zako, miongoni mwa dada zako, au mbele ya walimwengu. Ikiwa huwezi kuwa na ushuhuda mbele ya Shetani, Shetani atakucheka, atakuchukulia kama mzaha, mwanasesere, mara kwa mara atakuchezea na kukughadhibisha. Majaribu mengi yatakupata siku za usoni—lakini ikiwa leo unampenda Mungu kwa moyo wa dhati, na ikiwa haijalishi ukubwa wa majaribu yaliyo mbele, bila kujali unachokipitia, unaweza kusimama imara katika ushuhuda wako, na kuweza kumridhisha Mungu, basi moyo wako utafarijiwa, na utakuwa jasiri hata majaribu utakayokabiliana nayo siku za usoni

yawe makubwa kiasi gani. Hamwezi kuona ni nini kitatendeka siku za usoni; mnaweza tu kuridhisha Mungu katika hali ya leo. Hamwezi kufanya kazi yoyote kubwa, na unafaa kulenga kumridhisha Mungu kwa kuyapitia maneno yake katika maisha halisi, na kuwa na ushuhuda thabiti na mzito ambao unamtia aibu Shetani. Japo mwili wako hautaridhishwa na utateseka, utakuwa umemridhisha Mungu na kumletea aibu Shetani. Ikiwa daima unatenda hivi, Mungu atakufungulia njia mbele yako. Na siku moja, jaribio kubwa likija, wengine wataanguka chini, ila utaweza kuendelea kusimama imara: kwa sababu ya gharama uliyolipa, Mungu atakulinda ili usimame imara na usianguke. Kwa kawaida, ikiwa unaweza kuweka ukweli katika vitendo na kumridhisha Mungu kwa moyo ambao unampenda kweli, kwa hakika Mungu atakulinda wakati wa majaribu ya siku zijazo. Japokuwa wewe ni mpumbavu na mwenye kimo cha chini na usiye mwerevu, Mungu hatakubagua. Inategemea iwapo motisha zako ni za haki. Unaweza kumridhisha Mungu leo, iwapo uko makini na masuala madogo, unamridhisha Mungu kwa mambo yote, una moyo unaompenda Mungu kwa dhati, unampa Mungu moyo wa dhati, na japokuwa kuna baadhi ya mambo ambayo huwezi kuelewa, unaweza kwenda mbele za Mungu kurekebisha motisha zako, na kuyafuata mapenzi ya Mungu, na kufanya kila lipaswalo kumridhisha Mungu. Pengine ndugu na dada zako wataachana nawe, lakini moyo wako utakuwa unamridhisha Mungu, na hutatamani raha za mwili. Ikiwa daima unatenda kwa namna hii, utalindwa majaribu yakikusibu.

Majaribu haya yanailenga hali gani ya ndani ya watu? Yanalenga tabia ya uasi ndani ya watu ambayo haiwezi kumridhisha Mungu. Kuna mengi ambayo ni machafu ndani ya watu, na mengi ambayo ni ya unafiki, na kwa hivyo Mungu anawatia katika majaribu ili kuwasafisha. Lakini, ikiwa leo unaweza kumridhisha Mungu, basi majaribu ya siku zijazo yatakuwa ukamilifu kwako. Ikiwa leo, huwezi kumridhisha Mungu, basi majaribu ya siku za usoni yatakushawishi, na utaanguka bila kujua, na wakati huo hutaweza kujisaidia mwenyewe, kwani huendani na kazi ya Mungu, na huna kimo halisi. Na kwa hivyo, kama unataka kuweza kusimama imara katika siku za usoni, kumridhisha vyema Mungu, na kumfuata hadi mwisho, unapaswa kujenga msingi thabiti leo, unafaa kumridhisha Mungu kwa kutia ukweli katika vitendo kwa kila jambo, na kuzingatia mapenzi Yake. Iwapo daima unatenda kwa namna hii, kutakuwa na msingi ndani yako, na Mungu atahamasisha ndani yako moyo unaompenda, na Atakupa imani. Siku moja ambapo majaribu yatakuwa yamekukumba kwa kweli, ijapo utaumia, na kuhisi umedhulumiwa kwa kiwango fulani, na kuwa na huzuni kubwa, kana kwamba ulikuwa umekufa—ila mapenzi yako kwa Mungu hayatabadilika, na yataongezeka zaidi. Hizo ni baraka za Mungu. Ikiwa unaweza kumkubali Mungu na yote asemayo na atendayo leo kwa moyo mtiifu, basi kwa hakika utabarikiwa na Mungu, na kwa hivyo utakuwa mtu aliyebarikiwa na Mungu, na anayepokea ahadi Yake. Ikiwa leo hutendi, siku ambayo majaribu yatakukumba utakosa imani au moyo

wenye mapenzi, na wakati huo jaribu litakuwa kishawishi; utatoswa ndani ya kishawishi cha Shetani na hutapata namna ya kuponyoka. Leo, unaweza kusimama imara jaribio dogo likikukabili, ila huenda usiweze kusimama imara siku ambayo jaribio kubwa litakukumba. Baadhi ya watu hujivuna, na kufikiri kwamba wako karibu na ukamilifu. Ikiwa huzami zaidi wakati huo, na kuridhika, basi utakuwa hatarini. Leo, Mungu hafanyi kazi ya majaribu makubwa, kwa kuonekana, kila kitu kiko salama, ila Mungu atakapokujaribu, utagundua kuwa umepungukiwa sana, kwani kimo chako ni kidogo mno, na huna uwezo wa kustahimili majaribu mazito. Ukisalia jinsi ulivyo na uko katika hali ya inesha, basi, majaribu yatakapokuja, utaanguka. Mara nyingi inafaa mtazame udogo wa kimo chenu; mtapiga hatua kwa njia hii tu. Ikiwa unauona udogo wa ukomavu wako wakati wa majaribu tu, kwamba kimo chako ni dhaifu, kwamba kuna kidogo sana ndani yako ambacho ni halisi, na kwamba hutoshi kwa mapenzi ya Mungu—na kama utagundua haya wakati wa majaribu tu, utakuwa umechelewa mno.

Ikiwa hujui tabia ya Mungu, bila shaka utaanguka wakati wa majaribu, kwa kuwa hufahamu jinsi Mungu anavyowafanya watu kuwa wakamilifu, na ni kwa njia gani Huwafanya wakamilifu, na majaribu ya Mungu yakikushukia na yasilingane na mawazo yako, utashindwa kusimama imara. Upendo wa kweli wa Mungu ni tabia Yake kamili, na tabia kamili ya Mungu inapoonyeshwa kwa watu, hili linauletea mwili wako nini? Tabia ya haki ya Mungu inapoonyeshwa kwa watu, bila shaka miili yao iapata uchungu mkubwa zaidi. Iwapo hutapata haya maumivu, basi huwezi kufanywa mkamilifu na Mungu, wala huwezi kumpa Mungu mapenzi ya kweli. Mungu akikufanya mkamilifu kwa hakika atakuonyesha tabia Yake kamili. Tangu uumbaji hadi leo, Mungu hajawahi kumwonyesha mwanadamu tabia Yake kamili—ila katika siku za mwisho Anaifichua kwa hili kundi la watu ambao Aliwateua awali na kuwachagua, na kwa kuwafanya watu wakamilifu, Anaiweka wazi tabia Yake, na kupitia kwayo Analifanya kamili kundi la watu. Huo ndio upendo wa kweli wa Mungu kwa watu. Kuyapitia mapenzi ya kweli ya Mungu kunawapasa watu wastahimili uchungu mkali, na kulipa gharama kubwa. Ni baada tu ya hili ndipo watapatikana na Mungu na waweze kutoa tena mapenzi ya kweli kwa Mungu, na ni hapo tu ndipo Moyo wa Mungu utaridhishwa. Ikiwa watu wanataka wafanywe wakamilifu na Mungu, na kama wanataka kufanya na mapenzi Yake, na kumpa Mungu mapenzi yao ya dhati kikamilifu, ni sharti wapitie mateso mengi na maumivu makali kutokana na hali hizo, kupata uchungu mkali kuliko mauti, hatimaye watashurutishwa kuirejesha mioyo yao ya kweli kwa Mungu. Ikiwa mtu anampenda Mungu kwa dhati au la, itafichuliwa wakati wa shida na usafishaji. Mungu hutakasa mapenzi ya watu, na hili vilevile hupatikana tu ndani ya shida na usafishaji.

Mazungumzo Mafupi Kuhusu “Ufalme wa Milenia Umefika”

Mnayaonaje maono ya Ufalme wa Milenia? Baadhi ya watu hutafakari sana kuuhusu na kusema kuwa Ufalme wa Milenia utadumu duniani kwa miaka elfu moja, hivyo basi ikiwa waumini wazee katika kanisa hawajaoa, je, wanapaswa kuoa? Familia yangu haina pesa, je napaswa nianze kutafuta pesa? ... Ufalme wa Milenia ni nini? Je, mnajua? Watu ni nusu vipofu na wanapitia mateso mengi. Kwa hakika, Ufalme wa Milenia bado haujafika rasmi. Katika hatua ya kuwafanya wanadamu wakuwe wakamilifu, Ufalme wa Milenia bado hauna uzoefu; katika kipindi cha Ufalme wa Milenia uliozungumziwa na Mungu, mwanadamu atakuwa amefanywa mkamilifu. Hapo nyuma, ilisemekana kwamba watu wangekuwa kama watakatifu na kusimama imara katika nchi ya Sinimu. Ni pale tu watu watakapofanywa wakamilifu—watakapokuwa watakatifu walionenwa na Mungu—ndipo Ufalme wa Milenia utakapokuwa umefika. Mungu anapowafanya watu kuwa wakamilifu, anawatakaswa, na kadiri walivyo wasafi ndivyo wanavyofanywa wakamilifu na Mungu. Uchafu, uasi, upinzani na mambo ya kimwili yakitokomezwa kutoka kwako, ukishatakaswa, basi utakuwa mpendwa wa Mungu (na kwa maneno mengine, utakuwa mtakatifu); ukifanywa mkamilifu na Mungu na kuwa mtakatifu, utakuwemo katika Ufalme wa Milenia. Sasa ni Enzi ya Ufalme. Katika Enzi ya Ufalme wa Milenia, watu watategemea maneno ya Mungu kuishi, na mataifa yote yatakuja chini ya jina la Mungu, na wote watapata kusoma maneno ya Mungu. Wakati huo, wengine watapiga simu, na wengine watatuma faksi ... watatumia kila njia kuyafikia maneno ya Mungu, nanyi, vilevile, pia, mtakuja chini ya maneno ya Mungu. Haya yote ni maswala yanayofanyika baada ya watu kufanywa wakamilifu. Leo hii, watu wanafanywa wakamilifu, wanasafishwa, wanapata nuru, na kuongozwa kupitia kwa maneno; hii ni Enzi ya Ufalme, ni hatua ya watu kufanywa wakamilifu na haina uhusiano na Enzi ya Ufalme wa Milenia. Wakati wa Enzi ya Ufalme wa Milenia, watu tayari watakuwa wamefanywa wakamilifu, na tabia mbovu ndani yao zitakuwa zimetakaswa. Wakati huo, maneno yasemwayo na Mungu yatawaongoza wanadamu hatua kwa hatua, na kufichua siri za kazi ya Mungu tangu uumbaji hadi leo, na maneno Yake yatawaambia watu kuhusu matendo ya Mungu katika kila enzi na kila siku, jinsi Anavyowaongoza watu ndani, kazi Aifanyayo katika ufalme wa kiroho, na yatawaambia kuhusu mienendo ya ufalme wa kiroho. Hapo tu ndipo itakuwa Enzi ya kikweli ya Neno; kwa sasa iko tu katika hali isiyo na uzoefu tu. Iwapo watu hawatafanywa wakamilifu na kutakaswa, hawatakuwa na njia ya kuishi miaka elfu moja duniani, na miili yao pasi kuzuia itaoza; iwapo watu watatakaswa kwa ndani, na kamwe wasiwe wa Shetani na wa kimwili, basi watabaki hai duniani. Katika hatua hii, bado uko nusu kipofu na yote unayoyapitia ni Mungu wa upendo na kuwa na ushuhuda Kwake kila siku mnayoishi duniani.

“Ufalme wa Milenia Umefika” ni unabii, ni mfano wa utabiri wa nabii ambao kwao Mungu anatabiri kitakachofanyika hapo mbeleni. Maneno anenayo Mungu siku za usoni na yale

Anayoyanena leo hii si sawa: Maneno ya siku za usoni yataiongoza enzi, ilhali maneno anenayo leo hii yanawafanya watu kuwa wakamilifu, kuwasafisha na kuwashughulikia. Enzi ya Neno katika siku zijazo ni tofauti na Enzi ya Neno leo. Leo, maneno yote yanenwayo na Mungu—bila kujali Ameyanena kwa namna gani—kwa ujumla, ni kwa ajili ya kuwafanya watu kuwa wakamilifu, kutakasa kile kilicho kichafu ndani yao, na kuwafanya watakatifu na wenye haki mbele ya Mungu. Maneno yanenwayo leo na maneno yatakayonenwa katika siku za usoni ni vitu viwili tofauti. Maneno yanenwayo katika Enzi ya Ufalme ni ya kuwafanya watu waingie katika mafunzo yote, kuwafanya watu waingie katika njia sahihi kwa kila kitu, kukitokomeza chochote kilicho kichafu ndani yao. Hayo ndiyo Mungu Anayofanya katika enzi hii: Anajenga msingi wa maneno Yake kwa kila mtu, Anayafanya maneno Yake kuwa uzima wa kila mtu na Anayatumia maneno Yake kuwapatia nuru watu na kuwaongoza ndani kila wakati, na wasipoyajali mapenzi ya Mungu, maneno ya Mungu yatakuwa ndani yao kuwakemea na kuwafundisha nidhamu. Maneno ya leo yanafaa kuwa uzima wa mwanadamu, yanatoa moja kwa moja kila anachokihitaji mwanadamu, kila unachokikosa kwa ndani kinatolewa na maneno ya Mungu, na wale wote wanaoyakubali maneno ya Mungu wanapata nuru kwa kula na kunywa maneno Yake. Maneno yanenwayo na Mungu katika siku za usoni huwaongoza watu wa ulimwengu mzima; leo hii, maneno haya yanazungumzwa Uchina pekee, na hayawakilishi yale yanenwayo ulimwenguni kote. Mungu Atazungumza tu na ulimwengu mzima Ufalme wa Milenia ukija. Fahamu kuwa maneno yanenwayo na Mungu leo hii ni kuwafanya watu kuwa wakamilifu; maneno yanenwayo na Mungu katika hatua hii ni ya kuwapa watu mahitaji yao, si ya kukufanya ujue siri au kuiona miujiza ya Mungu. Kunena kwake kwa namna nyingi ni ili awapatie watu mahitaji yao. Enzi ya Ufalme wa Milenia haujafika bado—Enzi ya Ufalme wa Milenia inayozungumziwa ni siku ya utukufu wa Mungu. Baada ya kazi ya Yesu kule Uyahudi kukamilika, Mungu Aliihamishia kazi yake barani Uchina na kutengeneza mpango mwingine. Anaifanyia sehemu nyingine ya kazi Yake ndani yenu, Anafanya kazi ya kuwafanya watu wakamilifu kwa maneno, na kutumia maneno kuwafanya watu wapitie maumivu makali sana na pia kupata neema ya Mungu. Hii hatua ya kazi itaunda kundi la washindi na baada ya kuliunda kundi hili la washindi, wataweza kushuhudia matendo Yake, wataweza kuishi kwa kudhihirisha uhalisia, na kumtosheleza na kuwa waaminifu Kwake hadi kifo, na kwa njia hii Mungu Atatukuzwa. Mungu anapotukuzwa Atakapolifanya hili kundi la watu kuwa wakamilifu, itakuwa Enzi ya Ufalme wa Milenia.

Yesu Alikuwa duniani kwa miaka thelathini na tatu na nusu, Alikuwa kufanya kazi ya usulubisho na kupitia usulubisho, Mungu Alipata sehemu moja ya utukufu. Mungu Alipokuja katika mwili, Aliweza kunyenyekea na kujificha, na Aliweza kustahimili mateso makubwa. Japokuwa Alikuwa Mungu Mwenyewe, bado Alipitia kila aina ya fedheha, na kila aina ya matusi, na Alipitia uchungu mkubwa kwa kuangikwa msalabani ili kukamilisha kazi ya

ukombozi. Baada ya hatua hii ya kazi kutamatishwa, japokuwa watu waliona kuwa Mungu Alikuwa Amepata utukufu mkubwa, huu haukuwa ukamilifu wa utukufu Wake; ilikuwa tu sehemu moja ya utukufu Wake ambao Alikuwa Amepata kutoka kwa Yesu. Japokuwa Yesu Aliweza kupitia magumu ya kila aina, kuwa Mnyenyekevu na kujificha, kusulubishwa kwa ajili ya Mungu, Mungu Alipata tu sehemu moja ya utukufu Wake, na utukufu Wake ulipatikana Israeli. Mungu bado Ana sehemu nyingine ya utukufu: kuja duniani kufanya kazi na kufanya kundi la watu kuwa wakamilifu. Wakati wa hatua ya kazi ya Yesu, Alifanya baadhi ya mambo ambayo si ya kawaida, ila ile hatua ya kazi kwa yoyote ile haikuwa tu ili kufanya ishara na maajabu. Kimsingi ilikuwa kuonyesha kuwa Yesu Angeweza kuteseka na kusulubishwa kwa ajili ya Mungu, kwamba Yesu Angeweza kupitia uchungu mkubwa kwa kuwa Alimpenda Mungu, na kwamba japokuwa Mungu Alimtelekeza, bado Alikuwa radhi kuyatoa maisha Yake kwa ajili ya mapenzi ya Mungu. Baada ya Mungu kukamilisha kazi Yake Israeli na Yesu Kuangikwa msalabani, Mungu Alitukuzwa, na Mungu Alikuwa na ushuhuda mbele ya Shetani. Hamjui na wala hamjaona jinsi Mungu Amekuwa mwili nchini Uchina, basi mnaonaje kuwa Mungu Ametukuzwa? Mungu Anapofanya kazi nyingi ya ushindi kwenu, na mnasimama imara, basi hii hatua ya kazi ya Mungu inakuwa ya mafanikio, na hii ni sehemu ya utukufu wa Mungu. Mnaliona hili tu na bado hamjafanywa na Mungu kuwa wakamilifu, bado hamjaitoa roho yenu kwa Mungu kikamilifu. Bado hamjauona huu utukufu kwa ukamilifu; mnaona tu kwamba Mungu Ameushinda moyo wenu tayari, kwamba hammuachi kamwe na kwamba mtamfuata Mungu mpaka mwisho na moyo wenu hautabadilika, na huo ndio utukufu wa Mungu. Ni katika kitu gani mnauona utukufu wa Mungu? Kwenye athari za kazi Yake kwa wanadamu. Watu huona kuwa Mungu anapendeza sana, wana Mungu mioyoni mwao, na hawako radhi kumuacha, na huu ni utukufu wa Mungu. Wakati ambapo uthabiti wa ndugu na dada wa makanisa unapotokea, na wanaweza kumpenda Mungu kutoka mioyoni mwao, na kuuona ukuu wa kazi inayofanywa na Mungu, ukuu usiomithilika wa maneno Yake, waonapo kwamba maneno yake yanabeba mamlaka na kwamba anaweza kuanzisha kazi Yake katika miji iliyohamwa katika bara ya Uchina, wakati ambapo, japo watu ni wanyonge, mioyo yao inasujudu mbele ya Mungu na wako radhi kuyakubali maneno ya Mungu, na wakati ambapo, japo ni wanyonge na wasiofaa, wanaweza kuona kuwa maneno ya Mungu ni ya kupendeza sana na yastahili utunzaji wao basi huu ndio utukufu wa Mungu. Siku ikija ambayo watu watafanywa wakamilifu na Mungu, na wanaweza kujisalimisha mbele Yake, na kuweza kumtii Mungu kabisa, na kuyawacha matarajio na majaliwa yao mikononi mwa Mungu, basi sehemu ya pili ya utukufu wa Mungu itakuwa imepatikana kikamilifu. Hii ni kusema kuwa wakati ambapo kazi ya Mungu wa vitendo itakapokuwa imekamilishwa kabisa, kazi Yake katika bara ya Uchina itafika kikomo; kwa maneno mengine, wakati wale walioamuliwa kabla na kuchaguliwa na Mungu watakapokuwa wamefanywa wakamilifu, Mungu Atatukuzwa. Mungu Alisema kwamba Ameleta sehemu ya pili

ya utukufu Wake Mashariki, na bado hili halionekani kwa macho. Mungu Ameleta kazi Yake Mashariki: tayari Amekuja Mashariki, na huu ni utukufu wa Mungu. Leo ingawa kazi yake haijakamilika bado, kwa sababu Mungu Ameamua kufanya kazi, bila shaka itakamilika. Mungu Ameamua kuwa Ataikamilishia kazi yake Uchina, na Ameamua kuwafanya kuwa wakamilifu. Hivyo Hawapatii njia nyingine—tayari Ameishinda mioyo yenu, na lazima utaendelea upende usipende, na mnapokubaliwa na Mungu, Mungu Anatukuzwa. Leo hii bado Mungu Hajatukuzwa kikamilifu, kwa sababu bado hujafanywa kuwa wakamilifu. Ingawa moyo wako umerudi kwa Mungu, bado kuna udhaifu mwingi katika mwili wako, hauna uwezo wa kumridhisha Mungu, huwezi kushughulishwa na mapenzi ya Mungu, na bado mna vitu vingi hasi ambavyo ni sharti muondokane navyo nab ado lazima mpitie majaribu na usafishaji mwingi. Ni kwa njia hiyo tu ndiyo tabia zenu za maisha zinaweza kubadilika na mnaweza kupatwa na Mungu.

Wale Wanaomjua Mungu Pkee Ndio Wanaoweza Kuwa na Ushuhuda Kwa Mungu

Ni sheria ya Mbinguni na kanuni za duniani kumwamini Mungu na kumjua Mungu, na leo—wakati wa enzi ambapo Mungu mwenye mwili Anafanya kazi Yake mwenyewe—ndio wakati mwafaka hasa wa kumjua Mungu. Kumridhisha Mungu kunaafikiwa kwa msingi wa kufahamu mapenzi ya Mungu, na kuyafahamu mapenzi ya Mungu, ni muhimu kumjua Mungu. Ufahamu huu wa Mungu ni maono ambayo muumini anapaswa kuwa nayo; huu ndio msingi wa imani ya mwanadamu katika Mungu. Iwapo mwanadamu hana ufahamu huu, basi imani yake katika Mungu si dhahiri, na imejengwa juu ya nadharia tupu. Ingawa ni uamuzi wa watu kama hawa kumfuata Mungu, hawafaidi chochote. Wale wote wasiopata chochote kwenye mkondo huu ndio watakaondolewa—wao wote hawana kazi. Haijalishi ni hatua gani ya kazi ya Mungu unayopitia, lazima uandamane na maono makuu. Bila maono kama haya, itakuwa vigumu kwako kukubali kila hatua ya kazi mpya, kwa maana mwanadamu hana uwezo wa kuwaza kuhusu kazi mpya ya Mungu, ni kuu kushinda mawazo ya mwanadamu. Kwa hivyo bila mchungaji kumlinda mwanadamu, bila mchungaji kushirikiana na mwanadamu kuhusu maono hayo, mwanadamu hana uwezo kukubali kazi hii mpya. Iwapo mwanadamu hawezi kupokea maono haya, basi hawezi kupata kazi mpya ya Mungu, na iwapo mwanadamu hawezi kutii kazi mpya ya Mungu, basi mwanadamu hana uwezo wa kuyaelewa mapenzi ya Mungu, na hivyo ufahamu wake wa Mungu ni bure. Kabla mwanadamu atimilize maneno ya Mungu, lazima ayajue maneno ya Mungu, hivyo ni kusema, aelewe mapenzi ya Mungu; ni kwa njia hii tu ndiyo maneno ya Mungu yanaweza kutekelezwa kwa usahihi na kulingana na moyo wa Mungu. Hili lazima liwe na kila mmoja anayetafuta ukweli, na ndiyo njia ambayo lazima kila mmoja anayejaribu kumjua Mungu aipitie. Njia ya kuyajua maneno ya Mungu ndiyo njia ya kumjua Mungu, na pia njia ya kuijua

kazi ya Mungu. Na hivyo, kujua maono hakuashirii tu kuujua ubinadamu wa Mungu mwenye mwili, lakini pia kunajumuisha kujua maneno na kazi ya Mungu. Kutokana na maneno ya Mungu wanadamu wanapata kuelewa mapenzi ya Mungu, na kutokana na maneno ya Mungu wanapata kuelewa tabia ya Mungu na pia kujua kile Mungu alichok. Imani katika Mungu ndiyo hatua ya kwanza katika kumjua Mungu. Harakati ya kusonga kutoka katika imani ya mwanzo katika Mungu mpaka imani kuu kwa Mungu ndiyo njia ya kumjua Mungu, na harakati ya kuipitia kazi ya Mungu. Iwapo unaamini kwa Mungu kwa ajili tu ya kuamini kwa Mungu, na huamini kwa Mungu kwa ajili ya kumjua Mungu, basi hakuna ukweli katika imani yako, na haiwezi kuwa safi—kuhusu hili hakuna tashwishi. Iwapo, wakati wa harakati anapopata uzoefu wa kazi ya Mungu mwanadamu anapata kumjua Mungu polepole, basi hatua kwa hatua tabia yake itabadilika pia, na imani yake itaongezeka kuwa ya kweli zaidi. Kwa njia hii, wakati mwanadamu anafaulu katika imani yake kwa Mungu, ataweza kumpata Mungu kwa ukamilifu. Mungu alijitoa pakubwa kuingia katika mwili mara ya pili na kufanya kazi Yake binafsi ili mwanadamu apate kumjua Yeye, na ili mwanadamu aweze kumwona. Kumjua Mungu^[a] ndiyo matokeo ya mwisho yanayofikiwa katika mwisho wa kazi ya Mungu; ndilo hitaji la mwisho la Mungu kwa mwanadamu. Anafanya hili kwa ajili ya ushuhuda Wake wa mwisho, na ili kwamba mwanadamu mwishowe na kwa kikamilifu aweze kumgeukia Yeye. Mwanadamu anaweza tu kumpenda Mungu kwa kumjua Mungu, na ili ampende Mungu lazima amjue Mungu. Haijalishi vile anavyotafuta, au kile anachotafuta kupata, lazima aweze kupata ufahamu wa Mungu. Ni kwa njia hii tu ndiyo mwanadamu anaweza kumridhisha Mungu. Ni kwa kumjua Mungu tu ndio mwanadamu anaweza kumwamini Mungu kwa ukweli, na ni kwa kumjua Mungu tu ndio anaweza kumwogopa na kumheshimu Mungu kwa kweli. Wale wasiomjua Mungu hawataweza kumwogopa na kumheshimu Mungu kwa kweli. Kumjua Mungu kunahusisha kujua tabia ya Mungu, kuelewa mapenzi ya Mungu, na kujua kile Mungu alichok. Na haijalishi ni kipengee gani cha kumjua Mungu, kila mojawapo kinamhitaji mwanadamu alipe gharama, na kinahitaji nia ya kutii, ambapo bila hivi hakuna atakayeweza kufuata mpaka mwisho. Kazi ya Mungu hailingani na mawazo ya mwanadamu hata kidogo, tabia ya Mungu na kile Mungu alichok ni vitu vigumu sana kwa mwanadamu kufahamu, na yote Anayosema na kufanya Mungu ni makuu sana yasiyoeleweka na mwanadamu; iwapo mwanadamu anatamani kumfuata Mungu, na hana nia ya kumtii Mungu, basi mwanadamu hatafaidi chochote. Tangu kuumbwa kwa dunia mpaka sasa, Mungu Amefanya kazi nyingi ambayo haieleweki na mwanadamu na ambayo mwanadamu amepata ugumu kuikubali, na Mungu amesema mengi yanayofanya mawazo ya mwanadamu magumu kupona. Ilhali Hajawahi kukomesha kazi Yake kwa sababu mwanadamu ana ugumu mwingi; Ameendelea kufanya kazi na kuzungumza, na hata ingawa idadi kubwa ya “wanajeshi” wameangamia njiani, Yeye bado Anaendelea na kazi Yake, na bado anateua kundi baada ya kundi la watu walio tayari kukubali kazi Yake mpya. Yeye hawahurumii wale “mashujaa”

walioangamia, na badala yake anawathamini wale wanaoikubali kazi Yake mpya na maneno. Lakini ni kwa sababu gani ndiyo Anafanya kazi kwa njia hii, hatua kwa hatua? Ni kwa nini Yeye hutumia mbinu za aina hii kila mara? Kusudi la kazi Yake ni ile wanadamu wapate kumjua, na ili waweze kutwaliwa na Yeye. Kanuni ya kazi Yake ni kufanya kazi kwa wale wanaoweza kutii kazi Anayofanya leo, na sio kufanya kazi kwa wale wanaotii kazi Yake ya zamani, na wanaipinga kazi Yake ya leo. Hii ndiyo sababu hasa Amewafuta na kuwaangamiza watu wengi.

Matokeo ya funzo la kumjua Mungu haliwezi kufikiwa kwa siku moja au mbili: Mwanadamu lazima apate uzoefu wa matukio mengi, apatie mateso, na awe na utiifu wa kweli. Kwanza kabisa, anza na kazi na maneno ya Mungu. Lazima uelewe kumjua Mungu kunajumuisha nini, jinsi ya kupata maarifa kuhusu Mungu, na jinsi ya kumwona Mungu katika matukio yako. Hili ndilo kila mtu lazima afanye wakiwa bado hawajamjua Mungu. Hakuna anayeweza kushika kazi na maneno ya Mungu kwa mara moja, na hakuna anayeweza kupata maarifa ya ukamilifu wa Mungu kwa muda mfupi. Kinachohitajika ni harakati mahususi ya matukio, na bila haya hakuna mwanadamu atakayeweza kumjua au kumfuata Mungu kwa kweli. Mungu Anapofanya kazi zaidi, ndivyo mwanadamu anavyozidi kumjua. Zaidi kazi ya Mungu inavyokinzana na mawazo ya mwanadamu, ndivyo ufahamu wa mwanadamu Kwake unavyofanywa upya na wenye kina kirefu. Iwapo kazi ya Mungu ingebaki milele bila kubadilika, basi mwanadamu angekuwa tu na ufahamu mdogo wa Mungu. Kati ya uumbaji na wakati wa sasa, vitu ambavyo Mungu alifanya wakati wa Enzi ya Sheria, Alichofanya wakati wa Enzi ya Neema, na kile Afanyacho wakati wa Enzi ya Ufalme: lazima ujue vizuri sana maono haya. Lazima mjue kazi ya Mungu. Ni baada tu ya kumfuata Yesu ndio Petro alipata kujua polepole kuhusu kazi ambayo Roho alifanya ndani ya Yesu. Alisema, “Kutegemea matukio ya mwanadamu hakutoshi kufukia ufahamu kamili wa Mungu; Lazima kuwe na mambo mengi kutoka kwa kazi ya Mungu ya kutusaidia kumjua Mungu.” Mwanzoni, Petro aliamini kuwa Yesu alitumwa na Mungu, kama mtume, na hakumwona Yesu kama Kristo. Wakati huu, alipoanza kumfuata Yesu, Yesu Alimuuliza, “Simoni, mwana wa Yona, je, utanifuata?” Petro alisema, “Ni lazima nimfuate yule aliyetumwa na Baba wa mbinguni. Lazima nimtambue yule aliyechaguliwa na Roho Mtakatifu. Nitakufuata Wewe.” Kutoka kwa maneno Yake, inaonekana wazi kuwa Petro hakuwa na ufahamu kumhusu Yesu; alikuwa ameyapitia maneno ya Mungu, alikuwa amejikabili mwenyewe, na pia alikuwa amepitia ugumu kwa ajili ya Mungu, ilhali hakujua kazi ya Mungu. Baada ya muda wa uzoefu, Petro aliona ndani ya Yesu matendo mengi ya Mungu, aliona vile Mungu anavyopendeza, na aliona uwepo wa Mungu ndani ya Yesu. Vilevile, aliona kuwa maneno ya Yesu hayangeweza kuzungumzwa na mwanadamu, na kwamba kazi Aliyofanya Yesu haingefanyika na mwanadamu. Katika maneno ya Yesu na matendo Yake,

zaidi ya hayo, Petro aliona wingi wa hekima ya Mungu, na kazi nyingi ya uungu. Wakati wa matukio yake, hakupata kujijua mwenyewe tu, ila alitilia maanani matendo ya Yesu, ambayo kutokana nayo aligundua mambo mengi mapya; kama vile, kwamba kulikuwa na maonyesho mengi ya Mungu wa matendo katika kazi ya Aliyofanya Mungu kupitia kwa Yesu, na kwamba maneno ya Yesu, matendo Yake, na jinsi Alivyoyachunga makanisa na kazi Aliyofanya ilitofautiana kabisa na mwanadamu wa kawaida. Hivyo, kutoka kwa Yesu Petro alijifunza mafunzo mengi aliyopaswa kusoma, na kufikia wakati Yesu Alikuwa karibu kusulubiwa, alikuwa amepata ufahamu kiasi kuhusu Yesu—ufahamu ambao ulikuwa msingi wa uaminifu wake wa maisha katika Yesu, na kusulubiwa kwake kichwa kikiwa chini ambako alipitia kwa ajili ya Bwana. Ingawa yeye alikuwa na fikira fulani na hakuwa na ufahamu kamili kuhusu Yesu mwanzoni, mambo kama haya bila shaka yanapatikana ndani ya wanadamu wapotovu. Alipokuwa karibu Anaondoka, Yesu Alimwambia Petro kwamba kusulubiwa Kwake ndiyo kazi Aliyokuja kufanya; Lazima Akataliwe na enzi hiyo, enzi hii nzee yenye uchafu lazima imsulubishe msalabani, na Alikuwa Amekuja kukamilisha kazi ya ukombozi, na, kwa kuwa Alikuwa ameikamilisha kazi hii, huduma Yake ilikuwa imekamilika. Aliposikia haya, Petro alipatwa na huzuni, na akampenda Yesu sana hata zaidi. Yesu Aliposulubiwa msalabani, Petro alilia kwa uchungu akiwa peke yake. Kabla ya hili, alikuwa amemuuliza Yesu, “Ee Bwana! Unasema kwamba unaenda kusulubiwa. Baada ya Wewe kwenda, tutakuona tena lini?” Je, hakuna mchanganyiko katika maneno Aliyozungumza? Je, hakuna fikira zake pale ndani? Moyoni mwake, alijua kuwa Yesu Alikuwa kukamilisha sehemu ya kazi ya Mungu, na kwamba baada ya Yesu kuondoka, Roho angekuwa pamoja naye; ingawa Angesulubiwa na Apae mbinguni, Roho wa Mungu Angekuwa pamoja naye. Wakati huo, alikuwa na ufahamu kiasi kumhusu Yesu, na kujua kwamba Alitumwa na Roho wa Mungu, kwamba Roho wa Mungu Alikuwa ndani Yake, na kwamba Yesu Alikuwa Mungu Mwenyewe, Alikuwa Kristo. Lakini kwa sababu ya upendo wake kwa Yesu, na kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu, bado Petro alisema maneno hayo. Ikiwa unaweza kutilia maanani na kupitia matukio ya hali ya juu katika kila hatua ya kazi ya Mungu, basi utaweza kuutambua uzuri wa Mungu hatua kwa hatua. Na maono ya Paulo yalikuwa yapi? Yesu Alipomwonekana, Paulo alisema, “Wewe ni nani, Bwana?” Yesu Akasema, “Mimi ndimi Yesu ambaye wewe unamtesa.” Haya ndiyo yalikuwa maono ya Paulo. Petro alitumia kufufuka kwa Yesu na kuonekana Kwake kwa siku arubaini, na mafunzo ya Yesu wakati wa maisha Yake, kama maono yake mpaka alipofika mwisho wa safari yake.

Mwanadamu hutambua kazi ya Mungu, hupata kujijua mwenyewe, hujitoa katika tabia yake potovu, na kutafuta kukua katika maisha yote kwa ajili ya kumjua Mungu. Ukitafta kujijua mwenyewe tu na kujishughulisha tu na tabia yako potovu, na huna ufahamu ni kazi gani Mungu

Anafanya kwa mwanadamu, kuhusu jinsi wokovu Wake ulivyo mkuu, au jinsi unavyojua kazi ya Mungu na kushuhudia matendo Yake, basi matukio yako hayana maana. Iwapo unafikiri kuwa kuweza kuuweka ukweli katika matendo, na kuwa na uwezo wa kuvumilia kunamaanisha maisha ya mtu yamekua, basi hii ina maana kuwa bado huelewi maana kamili ya Maisha au huelewi kusudi la Mungu la Kufanya kazi ya kumkamilisha mwanadamu. Siku moja, ukiwa katika makanisa ya kidini, miongoni mwa wanachama wa Kanisa la Toba au Kanisa la Uzima, utakutana na watu wengi wenye imani ambao maombi yao yana maono, na wanaohisi kuguzwa na walio na maneno ya kuwaongoza katika kuendelea kwao na maisha. Aidha, kwa mambo mengi wanaweza kuvumilia, na kujitelekeza wenyewe, bila kuongozwa na mwili. Wakati huo, hutaweza kujua tofauti: Utaamini kuwa kila wanachofanya ni sawa, kuwa ni udhihirisho wa kawaida wa maisha, lakini ni jambo la kusikitisha kweli kuwa jina wanaloamini si sahihi. Je imani kama hizi si pumbavu? Ni kwa nini inasemekana kuwa watu wengi hawana maisha? Ni kwa sababu hawamjui Mungu, na hivyo inasemekana kuwa hawana Mungu mioyoni mwao, na hawana uhai. Iwapo imani yako kwa Mungu imefikia kiwango fulani ambapo unaweza kwa kikamilifu kuyafahamu matendo ya Mungu, ukweli wa Mungu, na kila hatua ya kazi ya Mungu, basi umejawa na ukweli. Iwapo hujui kazi na tabia ya Mungu, basi uzoefu wako bado ni wa chini. Jinsi Yesu Aliifanya hatua ile ya kazi Yake, jinsi hatua hii inavyoendelezwa, jinsi Mungu Alifanya kazi Yake katika enzi ya Neema na ni kazi ipi iliyofanywa, ni kazi ipi inafanyika katika hatua hii—iwapo huna ufahamu kamilifu wa mambo haya, basi hutawahi kuondokewa na wasiwasi na utakuwa na shaka. Iwapo, baada ya kipindi cha uzoefu, wewe unaweza kujua kazi inayofanywa na Mungu na kila hatua ya kazi ya Mungu, na unao ufahamu mkuu wa malengo ya maneno ya Mungu, na ni kwa nini maneno mengi yaliyozungumzwa na Yeye hayajatimika bado, basi unaweza kutulia na kuendelea katika safari iliyo mbele yako, ukiwa huru kutokana na wasiwasi na kusafishwa. Mnapaswa kuona kile Mungu anatumia wingi wa kazi Yake. Yeye hutumia maneno Anayozungumza, akimsafisha mwanadamu na kuyabadilisha mawazo ya mwanadamu kupitia maneno mengi tofauti. Mateso yote ambayo mmestahimili, kusafishwa kote ambako mmepitia, kushughulikiwa ambako mmekukubali ndani yenu, kupata nuru ambako mmeona—yote yamefanikishwa kutumia maneno Aliyozungumza Mungu. Ni kwa sababu ya nini ndio mwanadamu anamfuata Mungu. Ni kwa sababu ya maneno ya Mungu! Maneno ya Mungu ni yenye mafumbo makuu, na yanaweza kuuguza moyo wa mwanadamu, kufunua vitu vilivyo ndani ya moyo wa mwanadamu, yanaweza kumfanya ajue vitu vilivyotendeka zamani, na kumruhusu kuona katika siku za usoni. Na kwa hivyo mwanadamu anavumilia mateso kwa sababu ya maneno ya Mungu, na anafanywa mkamilifu kwa sababu ya maneno ya Mungu, na ni baada ya hapo tu ndipo mwanadamu anamfuata Mungu. Anachostahili kufanya mwanadamu katika hatua hii ni kukubali maneno ya Mungu, na haijalishi kama amefanywa mkamilifu, au kusafishwa, kilicho cha muhimu ni maneno ya Mungu; hii ni kazi ya Mungu, na ni maono

ambayo mwanadamu lazima ayajue leo hii.

Mungu Anamfanyaje mwanadamu kuwa kamili? Tabia ya Mungu ni gani? Na ni nini kilicho ndani ya tabia Yake? Ili kuyabainisha mambo haya yote: mtu huliita kusambaza jina la Mungu, mtu huliita kuwa na ushuhuda kwa Mungu, na mtu huliita kumtukuza na kumsifu Mungu, na bila shaka mwanadamu atafikia mabadiliko katika tabia ya maisha yake kwa msingi wa kumjua Mungu. Kadri mwanadamu anavyopitia kushughulikiwa na kusafishwa, ndivyo nguvu yake inavyoongezeka zaidi, na hatua za Mungu zinavyozidi kuwa nyingi, ndivyo mwanadamu anavyofanywa kamili. Leo, katika uzoefu wa mwanadamu, kila hatua ya kazi ya Mungu inayagonga mawazo ya mwanadamu, na kila hatua haiwezi kuwazwa na akili ya mwanadamu, na kuzidi matarajio ya mwanadamu. Mungu Anakimu mahitaji yote ya mwanadamu, na kwa kila njia yote huwa yanakinzana na mawazo ya mwanadamu, na ukiwa mdhaifu, Mungu Ananena maneno Yake. Ni kwa njia hii tu ndio Anaweza kukupa uhai wako. Kwa kuzigonga fikira zako, unakuja kukubali kazi ya Mungu, na kwa njia hii pekee ndio unaweza kuondoa upotovu wako. Leo hii, kwa upande mmoja Mungu mwenye mwili Anafanya kazi katika uungu, na kwa upande mwingine Anafanya kazi katika ubinadamu wa kawaida. Unapoacha kuweza kukana kazi yoyote ya Mungu, unapoweza kutii bila kujali lolote Analosema Mungu au kufanya katika hali ya ubinadamu wa kawaida, unapoweza kutii na kuelewa bila kujali ni ukawaida wa aina gani Anadhihirisha: ni wakati huo tu ndio unaweza kuwa na uhakika kwamba Yeye ni Mungu, na ni hapo tu utakoma kuwa na dhana, na ni hapo tu ndio utaweza kumfuata mpaka mwisho. Kuna hekima katika kazi ya Mungu, na Anajua jinsi mwanadamu Anaweza kuwa na ushuhuda Kwake. Anajua pale ambapo udhaifu wa uhai wa mwanadamu upo, na maneno Anayozungumza yanaweza kukugonga pale penye udhaifu wako upo, lakini pia Anatumia maneno Yake makuu na yenye busara kukufanya uwe na ushuhuda Kwake. Hayo ndiyo matendo ya kimiujiza ya Mungu. Kazi inayofanywa na Mungu haiwezi kufikiriwa na akili ya mwanadamu. Hukumu ya Mungu inafunua aina za upotovu ambazo mwanadamu, kwa kuwa ni mwili, amejawa nao, na vitu vipi ndivyo umuhimu wa mwanadamu, na humwacha mwanadamu bila mahali pa kujificha aibu yake.

Mungu anafanya kazi ya hukumu na kuadibu ili kwamba mwanadamu amjue, na kwa ajili ya ushuhuda Wake. Bila hukumu Yake ya tabia potovu ya mwanadamu, basi mwanadamu hangeweza kujua tabia Yake ya haki isiyoruhusu kosa lolote, na hangeweza kubadili ufahamu Wake wa Mungu kuwa mpya. Kwa ajili ya ushuhuda Wake, na kwa ajili ya usimamizi Wake, Anafanya ukamilifu Wake kuwa wazi kwa kila mtu, hivyo kumwezesha mwanadamu kupata ufahamu wa Mungu, na kubadili tabia yake, na kuwa na ushuhuda mkuu kwa Mungu kupitia kuonekana kwa Mungu wa hadharani. Mabadiliko yanafanikishwa kwa tabia ya mwanadamu kupitia njia tofauti ya kazi ya Mungu; bila mabadiliko ya aina hii katika tabia ya mwanadamu,

mwanadamu hangeweza kuwa na ushuhuda kwa Mungu, na hangekuwa wa kuupendeza moyo wa Mungu. Mabadiliko katika tabia ya mwanadamu yanaashiria kwamba mwanadamu amejiweka huru kutokana na minyororo ya Shetani, amejiweka huru kutokana na ushawishi wa giza, na kwa kweli amekuwa mfano na kifaa cha kujaribiwa cha kazi ya Mungu, amekuwa shahidi wa kweli wa Mungu na mtu aliye wa kuupendeza moyo wa Mungu. Leo hii, Mungu mwenye mwili Amekuja kufanya kazi Yake duniani, na Anahitaji kwamba mwanadamu apate ufahamu kumhusu, aweze kumtii, awe na ushuhuda Kwake—aweze kujua kazi Yake ya matendo na ya kawaida, atii maneno Yake yote na kazi ambayo haiambatani na mawazo ya mwanadamu, na kuwa na ushuhuda kwa kazi Yake yote ya kumwokoza mwanadamu, na matendo yote Anayofanya ya kumshinda mwanadamu. Wale walio na ushuhuda kwa Mungu lazima wawe na ufahamu wa Mungu; ni aina hii tu ya ushuhuda ndio ulio sahihi, na wa kweli, na ni aina hii tu ya ushuhuda ndio unaoweza kumpa Shetani aibu. Mungu Anawatumia wale waliomjua baada ya kupitia hukumu Yake na kuadibu, ushughulikiaji na upogoaji, kuwa na ushuhuda Kwake. Anawatumia wale waliopotoshwa na Shetani kumtolea Yeye ushuhuda, na vilevile Anawatumia wale ambao tabia yao imebadilika, na wale basi ambao wamepokea baraka Zake, kumtolea ushuhuda. Yeye hana haja na mwanadamu kumsifu kwa maneno tu, wala hana hitaji lolote la sifa na ushuhuda kutoka kwa namna ya Shetani, ambao hawajaokolewa na Yeye. Ni wale tu wanaomjua Mungu ndio wanaohitimu kumtolea Mungu ushuhuda, na ni wale tu ambao tabia zao zimebadilika ndio wanaofaa kumshuhudia Mungu, na Mungu hatamruhusu mwanadamu kwa makusudi aliletee jina Lake aibu.

Tanbihi:

a. Nakala ya kwanza inasema “Kazi ya kumjua Mungu.”

Namna Petro Alivyopata Kumjua Yesu

Katika kipindi kile ambacho Petro alikuwa na Yesu, aliona sifa nyingi za kupendeza ndani ya Yesu, hali nyingi zenye za kustahili kuigwa, na nyingi ambazo zilimkimu. Ingawa Petro aliona nafsi ya Mungu ndani ya Yesu katika njia nyingi, na kuona sifa nyingi za kupendeza, mara ya kwanza hakumjua Yesu. Petro alianza kumfuata Yesu alipokuwa na umri wa miaka 20, na akaendelea kufanya hivyo kwa miaka sita. Katika kipindi hiki cha muda, hakuwahi kupata kumjua Yesu, lakini alikuwa radhi kumfuata kutokana na kuvutiwa na Yeye tu. Wakati Yesu alipomwita kwanza kwenye ufuko wa Bahari ya Galilaya, Aliuliza: “Simioni, mwana wa Yona, je, utanifuata?” Petro akasema: “Lazima nimfuate yeye aliyetumwa na Baba wa mbinguni. Lazima nimtambue yule aliyechaguliwa na Roho Mtakatifu. Nitakufuata.” Wakati huo, Petro alikuwa amesikia kuhusu mwanamume mmoja aliyetitwa Yesu, nabii mkubwa zaidi kuliko wote, Mwana mpendwa wa Mungu, na Petro alikuwa akitumai kila wakati kumpata, akitumai kupata

fursa ya kumwona Yeye (kwa sababu hivyo ndivyo alivyoongozwa wakati huo na Roho Mtakatifu). Ingawa alikuwa hajawahi kumwona Yeye na alikuwa amesikia tu uvumi kuhusu Yeye, kwa utaratibu tamanio na kivutio cha kumwabudu Yesu vyote vikaongezeka katika moyo wake, na mara nyingi alitamani siku ile atakayomtazama Yesu. Na Yesu alimwitaje Petro? Yeye pia alikuwa amesikia habari za mwanamume aliyeitwa Petro, na si kwamba Roho Mtakatifu alimwagiza: “Nenda katika Bahari ya Galilaya, pale ambapo kunaye bwana mmoja anayeitwa Simioni, mwana wa Yona.” Yesu alimsikia mtu akisema kwamba kulikuwa na bwana mmoja aliyeitwa Simioni, mwana wa Yona, na kwamba watu walikuwa wamesikia mahubiri yake, kwamba yeye pia alihubiri injili ya ufalme wa mbinguni, na kwamba watu waliomsikiliza waliguswa kiasi cha wote kutokwa na machozi. Baada ya kusikia haya, Yesu alimfuata mtu huyu, na kuelekea kwenye Bahari ya Galilaya; wakati Petro alipoukubali mwito wa Yesu, alimfuata.

Katika kipindi hiki akimfuata Yesu, Petro alikuwa na maoni mengi kuhusu Yeye na siku zote Alimhukumu kutokana na mtazamo wake. Ingawa alikuwa na kiwango fulani cha ufahamu wa Roho Mtakatifu, ufahamu huu haukuwa wazi kabisa, na haya yanaonekana katika maneno yake aliposema: “Lazima nimfuate yeye aliyetumwa na Baba wa mbinguni. Lazima nimtambue yule aliyechaguliwa na Roho Mtakatifu.” Hakuelewa mambo yale ambayo Yesu alifanya na hakuwa dhahiri kuyahusu. Baada ya kumfuata kwa muda fulani alivutiwa kwa kile alichofanya Yeye na kusema, na kwa Yesu Mwenyewe. Alikuwa kuhisi kwamba Yesu alivutia upendo na heshima; alipenda kujihusisha na Yeye na kuwa kando Yake, na kusikiliza maneno Yake Yesu kulimpa ruzuku na msaada. Katika kipindi kile alichomfuata Yesu, Petro alitazama na kutia moyoni kila kitu kuhusu maisha Yake: Matendo Yake, maneno Yake, mwendo Wake na maonyesho Yake. Alipata ufahamu wa kina kwamba Yesu hakuwa kama binadamu wa kawaida. Ingawa mwonekano Wake wa binadamu ulikuwa wa kawaida kabisa, Alijaa upendo, huruma, na ustahimilivu kwa binadamu. Kila kitu alichokifanya au kusema kilikuwa chenye msaada mkubwa kwa wengine, na akiwa kando Yake, Petro aliona na kujifunza mambo ambayo hakuwahi kuyaona wala kuyasikia awali. Aliona kwamba ingawa Yesu hakuwa na kimo kikubwa wala ubinadamu usio wa kawaida, Alikuwa na umbo la ajabu na lisilo la kawaida kwa kweli. Ingawa Petro hakuweza kuyafafanua kabisa, aliweza kuona kwamba Yesu alikuwa na mwenendo tofauti na kila mtu mwingine, kwani Aliyafanya mambo yaliyokuwa tofauti kabisa na yale yaliyofanywa na binadamu wa kawaida. Tangu wakati huo akiwa na Yesu, Petro alitambua pia kwamba hulka Yake ilikuwa tofauti na ile ya binadamu wa kawaida. Siku zote alikuwa na mwenendo dhabiti na hakuwahi kuwa na haraka, hakupigia chuku wala kupuuzwa chochote, na aliyaishi maisha Yake kwa njia iliyofichua hulka iliyokuwa ya kawaida na ya kuvutia. Katika mazungumzo, Yesu alikuwa mwenye madaha na uzuri, mwenye uwazi na mchangamfu ilhali pia

mtulivu, na Hakuwahi kupoteza heshima Yake katika utekelezaji wa kazi Yake. Petro aliona kwamba Yesu wakati mwingine alikuwa mnyamavu, ilhali nyakati nyingine alizungumza kwa mfululizo. Wakati mwingine Alikuwa na furaha sana kiasi kwamba alionekana kuwa njiwa anayerukaruka na kuchezeacheza, na ilhali nyakati nyingine Alihuzunika sana kiasi cha kwamba hakuzungumza kamwe, ni kana kwamba alikuwa mama aliyechoka sana. Nyakati nyingine Alijawa na hasira, kama askari jasiri anayefyatuka kuwaua adui, na wakati mwingine hata kama simba anayenguruma. Nyakati nyingine Alicheka; nyakati nyingine aliomba na kulia. Haijalishi ni vipi Yesu alivyotenda, Petro alizidi kuwa na upendo na heshima isiyokuwa na mipaka Kwake. Kicheko cha Yesu kilimjaza kwa furaha, huzuni Yake ikamtia simanzi, hasira Yake ikamtetemesha, huku huruma Zake, msamaha na madai makali Aliyotoa kwa watu yalimfanya aje kumpenda Yesu kwa kweli, na akaweza kumcha na kumtamani kwa kweli. Bila shaka, Petro alikuja kutambua haya yote kwa utaratibu baada ya kuishi kando yake Yesu kwa miaka michache.

Petro alikuwa ni binadamu mwenye akili, aliyekuwa na akili za asili, ilhali aliyafanya mambo mengi ya kijinga alipokuwa akimfuata Yesu. Mwanzoni kabisa, alikuwa na fikira fulani kuhusu Yesu. Aliuliza: “Watu wanasema kuwa Wewe ni nabii, kwa hiyo ulipokuwa na umri wa miaka minane na mkomavu vya kutosha kutambua mambo, je ulijua kuwa Wewe ni Mungu? Je ulijua kwamba mimba Yako ilitungwa na Roho Mtakatifu?” Yesu alijibu: “La, Sikujua. Kwani Sionekani kama mtu wa kawaida tu kwako? Mimi niko sawa na mtu yeyote mwingine yule. Yule mtu Baba hutuma ni mtu wa kawaida, na wala si mtu asiyekuwa wa kawaida. Na Ingawa kazi Ninayofanya inawakilisha Baba Yangu wa mbinguni, taswira Yangu, mtu Niliye, na mwili huu wa nyama haviwezi kuwakilisha kikamilifu Baba Yangu wa mbinguni—ni sehemu moja tu Yake. Ingawa Nilitoka kwenye Roho, Mimi Ningali mtu wa kawaida, naye Baba Yangu alinituma Mimi katika ulimwengu huu kama mtu wa kawaida, wala si mtu asiyekuwa wa kawaida.” Ni wakati tu Petro aliposikia haya ndipo alipopata ufahamu kidogo kuhusu Yesu. Na ilikuwa tu baada ya kupitia saa nyingi zisizohesabika za kazi ya Yesu, mafunzo Yake, uchungaji Wake, na ruzuku Yake, ndipo alipopata ufahamu wa kina zaidi. Katika mwaka Wake wa 30, Yesu alimwambia Petro kuhusu kusulubishwa Kwake kujako, kwamba Alikuwa amekuja kufanyahatua ya kazi—kazi ya kusulubishwa—ili kukomboa wanadamu wote. Alimwambia pia kwamba siku tatu baada ya kusulubishwa Kwake, Mwana wa Adamu angefufuka tena, na baada ya kufufuka Angeonekana kwa watu kwa siku 40. Baada ya kusikia maneno haya, Petro alikuwa na huzuni na kuathiriwa na maneno haya; kutoka hapo akawa karibu hata zaidi na Yesu. Baada ya kushuhudia mambo haya kwa muda fulani, Petro alikuja kutambua kwamba kila kitu Yesu alichofanya kilitokana na nafsi ya Mungu, na akaja kufikiria kwamba Yesu alikuwa wa kupendeka ajabu. Pale tu alipokuja kuwa na uelewa huu ndipo Roho Mtakatifu alimtia nuru

kutoka ndani yake. Kisha Yesu akawageukia wanafunzi wake na wafuasi wengine na kusema: “Yohana, wewe unasema Mimi ni nani?” Yohana akajibu: “Wewe ni Musa.” Kisha akamgeukia Luka: “Na wewe, Luka, wewe unasema Mimi ni nani?” Luka akajibu: “Wewe ndiwe mkubwa zaidi kati ya manabii.” Kisha akamwuliza mtawa na akajibu: “Wewe ndiwe nabii mkubwa zaidi anayeongea maneno mengi kutoka milele hadi milele. Hakuna unabii wa yeyote ulio mkubwa kama Wako, wala hakuna maarifa ya mtu yanayozidi Yako; Wewe ni nabii.” Kisha Yesu akamgeukia Petro na kuuliza: “Petro, wewe nawe unasema Mimi ni nani?” Petro akajibu: “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu Aliye hai. Unatoka mbinguni, Wewe si wa ulimwenguni, Wewe si sawa na viumbe wa Mungu. Sisi tuko ulimwenguni na Wewe u pamoja nasi hapa, lakini Wewe ni wa mbinguni, Wewe si wa ulimwengu, na Wewe si wa ulimwengu.” Ni kupitia katika uzoefu wake ndipo Roho Mtakatifu alipomtia nuru, hali iliyomwezesha kuwa na uelewa huu. Baada ya nuru hii, alivutiwa na kila kitu ambacho Yesu alikuwa amefanya hata zaidi, alimfikiria Yeye kuwa wa kupendeka hata zaidi, na siku zote alikuwa moyoni mwake asitake kutengana na Yesu. Kwa hiyo, mara ya kwanza Yesu alipojifichua kwake Petro baada ya kusulubishwa na kufufuka Petro alilia kwa furaha ya kipekee: “Bwana! Umefufuka!” Kisha, huku akilia, alimvua samaki mkubwa ajabu, akampika na kumpakulia Yesu. Yesu alitabasamu, lakini hakuongea. Ingawa Petro alijua Yesu alikuwa amefufuka, hakuelewa fumbo hilo. Alipompa Yesu samaki yule kumla, Yesu hakukataa na ilhali hakuongea wala kuketi chini kula, lakini badala yake alitoweka ghafla. Huu ulikuwa ni mshtuko wa ajabu kwake Petro, na hapo tu ndipo alipoelewa ya kwamba yule Yesu aliyefufuka alikuwa tofauti na yule Yesu wa awali. Baada ya kutambua hili, Petro alihuzunika, lakini pia akapata tulizo kwa kujua kwamba Bwana alikuwa amekamilisha kazi Yake. Alijua kwamba Yesu alikuwa amekamilisha kazi Yake, kwamba muda Wake wa kukaa na binadamu ulikuwa umeisha, na kwamba binadamu angelazimika kutembea kwa njia yake mwenyewe kuanzia hapo kuendelea. Yesu aliwahi kumwambia: “Lazima pia unywe kutoka kwenye kikombe kikali nilichonywea Mimi (hili ndilo alilomwambia baada ya kufufuka), lazima wewe pia utembe njia niliyotembea Mimi, lazima uyapoteze maisha yako kwa ajili Yangu.” Tofauti na sasa, kazi wakati huo haikuchukua mfumo wa mazungumzo ya uso kwa uso. Katika Enzi ya Neema, kazi ya Roho Mtakatifu ilikuwa fiche sana, naye Petro aliteseka katika ugumu mwingi, na wakati mwingine angefikia kiwango cha kumaka: “Mungu! Sina chochote ila maisha haya. Ingawa hayana thamani nyingi Kwako, ningependa kuyatoa Kwako. Ingawa binadamu hawastahili kukupenda, na upendo wao na mioyo yao haina thamani, naamini kwamba unajua hamu ya mioyo ya binadamu. Na hata ingawa miili ya binadamu haifikii ridhaa Yako, ningependa Wewe uweze kuukubali moyo wangu.” Baada ya kutamka maombi haya angetiwa moyo, haswa wakati alipoomba: “Niko tayari kuutoa moyo wangu wote kwa Mungu. Ingawa siwezi kumfanyia Mungu chochote, niko tayari kumtosheleza Mungu kwa utiifu na kujitolea Kwake kwa moyo wangu wote. Ninaamini Mungu lazima

auangalie moyo wangu.” Alisema: “Siombi chochote katika maisha yangu ila fikira zangu za upendo kwa Mungu na tamani la moyo wangu kuweza kukubaliwa na Mungu. Nilikuwa naye Bwana Yesu kwa muda mrefu, ilhali sikuwahi kumpenda Yeye, hili ndilo deni langu kubwa zaidi. Ingawa niliishi na Yeye, sikumjua, na hata nilisema mambo fulani ambayo hayakufaafaa kama Hayupo. Kufikiria kuhusu mambo haya kunanifanya kuhisi ni kana kwamba napaswa kumshukuru zaidi Bwana Yesu.” Siku zote aliomba kwa njia hii. Alisema: “Mimi ni duni kuliko vumbi. Siwezi kufanya chochote ila kuutoa moyo huu mtiifu kwa Mungu.”

Kulikuwepo na kilele katika yale Petro alipitia, wakati mwili wake ulikuwa karibu kunyenyekea kabisa, lakini Yesu akamtia moyo ndani. Na akajitokeza kwake mara moja. Wakati Petro alikuwa katika mateso makuu na kuhisi kwamba moyo wake ulisikitika, Yesu alimwelekeza: “Ulikuwa na Mimi ulimwenguni, na Nilikuwa na wewe hapa. Na Ingawa awali tulikuwa pamoja mbinguni, hata hivyo, ni ya ulimwengu wa kiroho. Sasa Nimerudi katika ulimwengu wa kiroho, na wewe umo ulimwenguni. Kwani Mimi si wa ulimwengu, na Ingawa wewe pia si wa ulimwengu, lazima utimize kazi yako hapa ulimwenguni. Kwani wewe ni mtumishi, lazima uwajibike kwa njia bora zaidi uwezayo.” Petro alipata tulizo, kwa kusikia kwamba angeweza kurudi kwa upande wa Mungu. Wakati Petro alipokuwa katika masumbuko hayo kiasi kwamba karibu awe mahututi kitandani, alisikitika kiasi cha kusema hivi: “Nimepotoka kwelikweli, siwezi kumtosheleza Mungu.” Yesu alijitokeza kwake na kusema: “Petro, huenda ikawa umesahau azimio ulilowahi kutoa mbele Yangu? Je, kwa kweli umesahau kila kitu Nilichosema? Umesahau azimio ulilonitolea?” Petro aliona kwamba alikuwa Yesu na akainuka kutoka kitandani, naye Yesu akamfariji: “Mimi si wa ulimwengu, tayari Nimekuambia wewe—hili lazima uelewe, lakini umesahau kitu kingine Nilichokuambia? ‘Wewe pia si wa ulimwengu, si wa dunia.’ Sasa hivi kunayo kazi unayohitaji kufanya, huwezi kuhuzunika namna hivi, huwezi kuteseka hivi. Ingawa binadamu na Mungu hawawezi kuishi pamoja katika ulimwengu mmoja, Ninayo kazi Yangu na wewe unayo yako, na siku moja wakati kazi yako imekamilika, tutakuwa pamoja katika himaya moja, nami Nitakuongoza wewe kuwa pamoja Nami milele na milele.” Petro alipata tulizo na hakikisho baada ya kuyasikia maneno hayo. Alijua kwamba kuteseka huku kulikuwa ni jambo ambalo lazima angevumilia na kupitia, na akatiwa msukumo kuanzia hapo kuendelea. Yesu alijitokeza haswa kwake katika kila muda muhimu, akimpa nuru na mwongozo maalum, na akifanya kazi nyingi ndani yake. Na ni nini ambacho Petro alijutia zaidi? Yesu alimwuliza Petro swali jingine (ingawa haijarekodiwa katika Biblia kwa njia hii) si kipindi kirefu baadaye Petro alikuwa amesema “Wewe ndiwe Mwana wa Mungu aliye hai,” nalo swali lenyewe lilikuwa: “Petro! Umewahi kunipenda?” Petro alielewa kile alichomaanisha, na kusema: “Bwana! Niliwahi kumpenda Baba wa mbinguni, lakini nakubali sijawahi kukupenda Wewe.” Yesu naye akasema: “Kama watu hawampendi Baba wa

mbinguni, watawezaje kumpenda Mwana hapa ulimwenguni? Na kama watu hawampendi Mwana aliyetumwa na Mungu, Baba, wanawezaje kumpenda Baba aliye mbinguni? Kama kweli watu wanampenda Mwana aliye ulimwenguni, basi kwa kweli wanampenda Baba aliye mbinguni.” Wakati Petro alipoyasikia maneno haya aligundua upungufu wake. Siku zote alihisi huzuni hadi kiwango cha kulia kutokana na maneno yake “niliwahi kumpenda Baba wa mbinguni, lakini sikuwahi kukupenda Wewe.” Baada ya ufufuo na kupaa angani kwa Yesu alihuzunika na kuwa na simanzi zaidi kwa yale yote yaliyokuwa yamefanyika. Huku akikumbuka kazi yake iliyopita na kimo chake cha sasa, mara nyingi angekuja mbele ya Yesu kwa maombi, siku zote akiwa na hisia za majuto na masikitiko kwa kutoweza kwake kutosheleza tamani la Mungu, na kutoweza kufikia viwango vya Mungu. Masuala haya yakawa ndiyo mzigo wake mkubwa. Alisema: “Siku moja nitatoa kila kitu nilicho nacho na kila nilicho, nitakupa kile chenye thamani zaidi.” Alisema: “Mungu! Ninayo imani moja tu na upendo mmoja tu. Maisha yangu hayana thamani, na mwili wangu hauna thamani. Ninayo imani moja tu na upendo mmoja tu. Ninayo imani kwako Wewe katika akili yangu na upendo Kwako wewe katika moyo wangu; mambo haya mawili tu ndiyo niliyonayo kukupatia Wewe, na wala sina kingine chochote.” Petro alihimizwa pakubwa na maneno yake Yesu, kwa sababu kabla ya Yesu kusulubishwa alikuwa amemwambia: “Mimi si wa ulimwengu huu, na wewe pia si wa ulimwengu huu.” Baadaye, wakati Petro alipofikia hali ya maumivu makali, Yesu alimkumbusha: “Petro, je, umesahau? Mimi si wa ulimwengu huu, na ni kwa ajili tu ya kazi Yangu ndipo Niliondoka mapema. Wewe pia si wa ulimwengu huu, umesahau? Nimekuambia mara mbili, kwani hukumbuki?” Petro alimsikia na kumwambia: “Sijasahau!” Yesu naye akasema: “Uliwahi kuwa na wakati mzuri ukiwa umekusanyika pamoja na Mimi kule mbinguni na kwa kipindi fulani kando Yangu mimi. Unanidata Mimi, na Mimi ninakudata. Ingawa viumbe hawa hawastahili kutajwa machoni Pangu, ninawezaje kukosa kupenda yule ambaye hana hatia na anapendeka? Je, umesahau ahadi Yangu? Lazima ulikubali agizo Langu hapa ulimwenguni, lazima utimize kazi Niliyokuaminia. Bila shaka siku moja Nitakuongoza kuwa kando Yangu.” Baada ya kuyasikia haya, Petro akahimizwa zaidi, na kupata msukumo mkubwa zaidi, kiasi cha kwamba alipokuwa msalabani, aliweza kusema hivi: “Mungu! Siwezi kukupenda vya kutosha! Hata ukiniomba nife, siwezi bado kukupenda vya kutosha! Popote Utakapotuma nafsi yangu, utimize au ukose kutimiza ahadi Zako za awali, chochote ufanyacho baadaye, ninakupenda na ninakuamini.” Kile alichoshikilia kilikuwa imani yake, na upendo wa kweli.

Jioni moja, wanafunzi mbalimbali, akiwemo Petro, walikuwa kwenye mashua ya kuvulia samaki. Walikuwa pamoja naye Yesu, naye Petro akamwuliza Yesu swali la kijinga sana: “Bwana! kunalo swali ambalo nimekuwa nalo kwa muda mrefu sana ambalo ningependa kukuuliza Wewe.” Yesu akajibu: “Basi uliza tafadhali!” Petro naye akauliza: “Je, kazi

iliyofanywa kwenye Enzi ya Sheria ilitokana na Wewe?” Yesu akatabasamu, kana kwamba alikuwa akisema: “Huyu mtoto, jinsi alivyo mjinga!” Kisha akaendelea kwa kusudio: “Haikuwa kazi Yangu hiyo, ilikuwa kazi ya Yehova na Musa.” Petro akasikia haya na kushangaa: “Salaale! Kwa hivyo haikuwa kazi Yako.” Punde tu Petro aliposema hayo, Yesu hakuongea tena. Petro akajiwazia: “Si Wewe uliyefanya kazi hiyo, kwa hiyo ndiyo maana umekuja kuiangamiza sheria, kwani hiyo haikuwa kazi Yako.” Moyo wake ukapata tulizo pia. Baadaye, Yesu akatambua kwamba Petro alikuwa mjinga kiasi, lakini kwa sababu hakuwa na utambuzi wowote wakati huo, Yesu hakusema chochote kingine au kumkemea waziwazi. Siku moja Yesu alihubiri kwenye sinagogi, palipokuwepo watu wengi, akiwemo Petro. Katika mahubiri Yake, Yesu alisema: “Yule atakayekuja kutoka milele hadi milele atafanya kazi ya ukombozi katika Enzi ya Neema, kuwakomboa wanadamu wote kutoka kwa dhambi, lakini, hatazuiliwa na taratibu zozote katika kumwongoza binadamu nje ya dhambi. Atatembea kutoka kwa sheria na kuingia katika Enzi ya Neema. Atakomboa wanadamu wote. Atapiga hatua mbele kutoka kwa Enzi ya Sheria hadi kwa ile Enzi ya Neema, ilhali hakuna atakayemjua Yeye, Yule aliyekuja kutoka kwa Yehova. Kazi aliyofanya Musa alipewa na Yehova; Musa aliziandika sheria kwa sababu ya ile kazi ambayo Yehova alikuwa amefanya.” Baada ya kusema hili, aliendelea: “Wale watakaotupilia mbali mafundisho ya Enzi ya Neema katika Enzi ya Neema watakumbana na janga. Lazima wasimame katika hekalu na kupokea maangamizo ya Mungu, nao moto utawajia.” Baada ya Petro kumaliza kusikiliza haya, alikuwa na mwitikio wa aina fulani na katika kipindi chote cha kile alichopitia Yesu alichunga na kumtunza Petro, huku akiongea naye kwa dhati, jambo ambalo lilimpatia Petro ufahamu bora zaidi kiasi kuhusu Yesu. Wakati Petro alipokuwa akifikiria kuhusu mahubiri ya Yesu ya siku hiyo, kisha swali alilowahi kumwuliza Yesu walipokuwa kwenye mashua ya kuvua samaki nalo jibu alilopewa na Yesu, pamoja na vile alivyocheke, ndipo alipoelewa kila kitu. Baadaye, Roho Mtakatifu alimtia nuru Petro, na kupitia kwa haya tu ndipo alipoelewa kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu aliye hai. Ufahamu wa Petro ulitokana na kutiwa nuru na Roho Mtakatifu, lakini kulikuwepo na mchakato katika uelewa huu. Ilikuwa kupitia kwa kuuliza maswali, kusikiliza mahubiri ya Yesu, kisha kupitia kupokea ushirika maalum wa Yesu na uchungaji Wake maalum, ndipo Petro alipokuja kutambua Yesu kuwa Mwana wa Mungu Aliye hai. Haya yote hayakufikiwa usiku kucha; ulikuwa ni mchakato, na huu ukawa ni msaada kwake katika yale yote aliyopitia baadaye. Kwa nini Yesu hakufanya kazi ya kukamilisha kwa watu wengine, lakini Petro tu? Kwa sababu Petro tu ndiye aliyelewa kwamba Yesu ndiye aliyekuja Mwana wa Mungu aliye hai na hakuna mwingine aliyejua hili. Ingawa kulikuwa na wanafunzi wengi waliojua mengi wakati walipomfuata, maarifa yao yalikuwa ya juujuu tu. Na ndiyo maana Petro alichaguliwa na Yesu kuwa mfano wa kukamilishwa. Kile Yesu alichomwambia Petro wakati huo ndicho anachowaambia watu leo, ambao maarifa yao na kuingia kwao katika maisha lazima yafikie yale ya Petro. Ni kulingana na mahitaji haya na njia

hii ndiyo Mungu atakapofanya kila mtu kuwa mkamilifu. Kwa nini watu leo wanahitajika kuwa na imani halisi na upendo wa kweli? Kile Petro alichopitia pia nyinyi lazima mpitie, yale matunda ambayo Petro alipata kutoka kwa yale aliyoyapitia pia lazima yaonyeshwe ndani yenu, na maumivu aliyoteseka Petro, nyinyi pia lazima mtayapitia kwa kweli. Njia mnayotembelea ndiyo ile ile ambayo Petro alitembelea. Maumivu mnayoteseka ndiyo maumivu ambayo Petro aliteseka. Mnapopokea utukufu na mnapoishi kwa kudhihirisha maisha halisi, basi mnaishi kwa kudhihirisha taswira ya Petro. Njia ni ileile, na kulingana na haya ndipo mtu anafanywa kuwa kamili. Hata hivyo, ubora wa tabia yenu kwa kiasi fulani unao upungufu ukilinganishwa na ule wa Petro, kwani nyakati zimebadilika, na ndivyo pia kiwango cha kupotoka. Na pia kwa Yudea kulikuwepo ufalme wa kipindi kirefu uliokuwa na utamaduni wa kale. Kwa hiyo lazima mjaribu kuboresha ubora wenu wa tabia.

Petro alikuwa mtu mwenye akili razini, mwerevu kwa kila kitu alichofanya, na pia mwaminifu kupindukia. Alikumbana na vipingamizi vingi. Alikumbana na jamii akiwa na umri wa miaka 14, huku akihudhuria shule na mara nyingi akienda kwenye sinagogi. Alikuwa na shauku nyingi na siku zote alikuwa radhi kuhudhuria mikutano. Wakati huo, Yesu alikuwa hajaanza rasmi kazi Yake; huu ulikuwa ni mwanzo tu wa Enzi ya Neema. Petro alianza kukumbana na wahusika wa kidini alipokuwa na umri wa miaka 14; kufikia wakati alipokuwa na umri wa 18 aliwasiliana na wajuzi wa kidini, lakini baada ya kushuhudia machafuko ya dini yaliyotendeka kisiri, aliondoka. Kwa kuona watu hao walivyokuwa wenye hila, wajanja, na waliojaa mabishano, aliudhika kabisa (hivi ndivyo Roho Mtakatifu alivyofanya kazi wakati huo, ili kumfanya kuwa mkamilifu. Roho Mtakatifu alimsukuma haswa na akaweza kufanya kazi maalum ndani yake), na hivyo basi akaondoka kwenye sinagogi akiwa na umri wa miaka 18. Wazazi wake walimtesa na wasingemruhusu kuamini (walikuwa wa shetani, na hawakuwa na imani yoyote). Hatimaye, Petro alitoka nyumbani na kusafiri kwa mapenzi yake, huku akivua samaki na kuhubiri kwa miaka miwili, kipindi ambacho aliweza pia kuwaongoza watu wachache kiasi. Sasa unafaa uweze kuona waziwazi njia iliyochukuliwa na Petro. Kama umeona hili waziwazi, basi utakuwa na hakika kuhusu kazi inayofanywa leo, kwa hiyo usingelalamika au kuwa kukaa tu, au kutamani chochote. Unafaa kupitia hali halisi aliyopitia Petro wakati huo: Alikumbwa na huzuni; hakuomba tena kuwa na mustakabali au baraka yoyote. Hakutafuta faida, furaha, umaarufu, au utajiri wa ulimwengu na alitafuta tu kuishi maisha yenye maana zaidi, ambayo yalikuwa ya kulipiza upendo wa Mungu na kujitolea kile alichokuwa nacho cha thamani kabisa kwa Mungu. Kisha angetosheka katika moyo wake. Mara nyingi aliomba kwa Yesu akitumia maneno haya: “Bwana Yesu Kristo, niliwahi kukupenda Wewe, lakini sikukupenda Wewe kwa kweli. Ingawa nilisema nina imani kwako Wewe, sikuwahi kukupenda kwa moyo wa kweli. Nilikuwa nakutazamia Wewe tu, nikikuabudu Wewe, na kukudata Wewe, lakini sikuwahi

kukupenda Wewe au kuwa na imani ya kweli kwako Wewe.” Siku zote aliomba ili kutoa azimio lake, alihimizwa kila wakati na maneno Yake Yesu na kuyageuza kuwa motisha. Baadaye, baada ya kipindi cha kile alichopitia, Yesu alimjaribu yeye, akimchochea kumtaka Yeye zaidi. Alisema: “Bwana Yesu Kristo! Ninakudata kweli, na kutamani kukutazamia. Ninakosa mengi mno, na siwezi kufidia upendo Wako. Ninakusihi kunichukua hivi karibuni. Utanihitaji mimi lini? Utanichukua lini? Ni lini nitakapoutazama uso Wako tena? Sitamani kuishi tena katika mwili huu, kuendelea kupotoka, na vilevile sitamani kuasi zaidi ya nilivyoasi. Niko tayari kujitolea vyote nilivyonavyo Kwako punde iwezekanavyo, na sitamani kukuhuzunisha Wewe zaidi ya hivi nilivyofanya.” Hivi ndivyo alivyoomba, lakini hakujua wakati huo kwamba Yesu angemfanya kuwa mkamilifu. Katika makali ya majaribio yake, Yesu alijitokeza kwake tena na kusema: “Petro, Ningependa kukufanya kuwa mkamilifu, ili uwe kipande cha tunda ambacho ni dhihirisho la Mimi kukukamilisha, ambacho Nitafurahia. Unaweza kweli kunishuhudia Mimi? Umefanya kile Nilichokuomba kufanya? Umeishi kwa kudhihirisha yale maneno Niliyoyaongea? Uliwahi kunipenda Mimi, lakini Ingawa ulinipenda Mimi, umeishi kwa kunidhihirisha? Ni nini ulichonifanyia Mimi? Unatambua kwamba wewe hufai upendo Wangu, lakini wewe umenifanyia nini?” Petro aliona kwamba alikuwa hajamfanyia Yesu chochote na akakumbuka kiapo cha awali cha kumpa Mungu maisha yake. Na kwa hiyo, hakulalamika tena, na maombi yake baadaye yakazidi kuwa bora zaidi. Akaomba, akisema: “Bwana Yesu Kristo! Niliwahi kukuacha Wewe, na Wewe pia uliwahi kuniacha mimi. Tumekuwa mbalimbali kwa kipindi cha muda, na muda kiasi tukiwa pia pamoja. Ilhali unanipenda mimi zaidi ya kila kitu kingine. Nimekuasi Wewe mara nyingi na nikakuhuzunisha mara nyingi. Ninawezaje kusahau mambo kama haya? Kazi uliyofanya ndani yangu mimi na kile ambacho umeniaminia nazingatia daima, sikisahau kamwe. Pamoja na kazi uliyonifanyia mimi nimejaribu kadri ya uwezo wangu. Unajua kile ninachoweza kufanya, na unajua zaidi wajibu ninaoweza kutekeleza. Ningependa kujitiisha kwa mipango Yako, na nitajitolea kila kitu nilicho nacho Kwako. Wewe tu ndiwe unayejua kile ninachoweza kukufanyia Wewe. Ingawa Shetani alinidanganya sana na nikakuasi Wewe, ninaamini kwamba Hunikumbuki mimi kwa ajili ya dhambi hizo, kwamba hunichukulii mimi kutokana na hizo dhambi. Ningependa kuyatoa maisha yangu yote kwa ajili Yako wewe. Siombi chochote, na wala sina matumaini au mipango mingine; ningependa tu kuchukua hatua kulingana na nia Zako na kutimiza mapenzi Yako. Nitakunywa kutoka kwenye kikombe Chako kichungu, na mimi ni Wako wa kuamuru.”

Lazima muwe wazi kuhusu njia mnayotembelea; lazima muwe wazi kuhusu njia mtakayotumia katika siku za usoni, ni nini haswa ambacho Mungu atafanya kuwa mkamilifu na ni nini ambacho mmeaminiwa nacho. Siku moja, pengine, mtajaribiwa, na kama wakati huo mtaweza kutiwa msukumo kutoka kwa yale aliyopitia Petro, yatawaonyesha kwamba kwa kweli

mnatembea njia ya Petro. Petro alipongezwa na Mungu kwa ajili ya imani na upendo wake wa kweli, na kwa ajili ya utiifu wake kwa Mungu. Na ilikuwa kutokana na uaminifu wake na kutamani kwake Mungu katika moyo wake ndiposa Mungu akamkamilisha kuwa timilifu. Kama kweli unao upendo na imani kama hiyo ya Petro, basi Yesu kwa kweli atakufanya kuwa timilifu.

Ni kwa Kupitia Usafishaji tu Ndiyo Mwanadamu Anaweza Kuwa na Upendo wa Kweli

Nyote mko katikati ya majaribu na usafishaji. Mnapaswa kumpendaje Mungu wakati wa usafishaji? Baada ya kupitia usafishaji, watu wanaweza kumtolea Mungu sifa ya kweli, na katika usafishaji, wanaweza kuona kwamba wamepungukiwa sana. Kadiri usafishaji wako ulivyo mkubwa, ndivyo unaweza zaidi kukana mwili; kadiri usafishaji wao ulivyo mkubwa, ndivyo zaidi ulivyo upendo wa watu kwa Mungu, Hili ndilo mnapaswa kuelewa. Je, kwa nini ni lazima watu wasafishwe? Linalenga kutimiza matokeo gani? Je, umuhimu wa kazi ya Mungu ya usafishaji kwa mwanadamu ni gani? Ukimtafuta Mungu kwa kweli, basi baada ya kupitia usafishaji Wake hadi kiwango fulani utahisi kwamba ni mzuri sana, na ni wa umuhimu mkubwa kabisa. Je, mwanadamu anapaswa kumpenda Mungu jinsi gani wakati wa usafishaji? Kwa kutumia azimio la kumpenda Mungu kukubali usafishaji Wake: Wakati wa usafishaji, unateseka ndani, kana kwamba kisu kinasokotwa moyoni mwako, ilhali uko tayari kumridhisha Mungu kwa kutumia moyo wako, ambao unampenda, na hauko tayari kuutunza mwili. Hii ndiyo maana ya kutenda upendo wa Mungu. Unaumia ndani, na mateso yako yamefikia kiwango fulani, lakini bado uko tayari kuja mbele ya Mungu na kuomba ukisema: “Ee Mungu! Siwezi kukuacha. Ingawa kuna giza ndani yangu, ningependa kukuridhisha; Unaujua moyo wangu, na ningependa kwamba Uwekeze zaidi ya upendo Wako ndani yangu.” Huu ndio utendaji wakati wa usafishaji. Ukitumia upendo wa Mungu kama msingi, usafishaji unaweza kukuleta karibu zaidi na Mungu na kukufanya mwandani zaidi wa Mungu. Kwa kuwa unamwamini Mungu, ni lazima uukabidhi moyo wako mbele ya Mungu. Ukiutoa moyo wako na kuuweka mbele ya Mungu, basi wakati wa usafishaji, haitawezekana wewe kumkana Mungu, au kumwacha Mungu. Kwa njia hii, uhusiano wako na Mungu utakuwa wa karibu hata zaidi, na wa kawaida hata zaidi, na mawasiliano yako na Mungu yatakuwa ya mara kwa mara zaidi. Ikiwa wewe daima hutenda kwa jinsi hii, basi utashinda wakati zaidi katika mwanga wa Mungu, na wakati zaidi chini ya mwongozo wa maneno Yake, kutakuwa pia na mabadiliko zaidi na zaidi katika tabia yako, na ufahamu wako utaongezeka kila siku. Siku itakapokuja na majaribu ya Mungu yakufike kwa ghafla, hutaweza tu kusimama kando ya Mungu, bali pia utaweza kuwa na ushuhuda kwa Mungu. Wakati huo, utakuwa kama Ayubu, na Petro. Baada ya kuwa na ushuhuda kwa Mungu, utampenda kwa kweli, na utamtotea maisha yako kwa furaha; utakuwa shahidi wa Mungu, na yule ambaye ni

mpendwa wa Mungu. Upendo ambao umepitia usafishaji ni wa nguvu, na sio dhaifu. Haijalishi ni lini au vipi Mungu anakufanya upatwe na majaribu Yake, unaweza kutojali ikiwa unaishi au unaangamia, kuachana na kila kitu kwa furaha kwa ajili ya Mungu, na kuvumilia chochote kwa furaha kwa ajili ya Mungu—na hivyo upendo wako utakuwa safi, na imani yako halisi. Ni hapo tu ndipo utakuwa mtu anayependwa na Mungu kwa kweli, na ambaye amefanywa kamili na Mungu kwa kweli.

Watu wakijipata chini ya ushawishi wa Shetani, basi hawana upendo kwa Mungu ndani yao, na maono, upendo na azimio yao ya awali yamepotea. Watu walikuwa wakihihi kwamba walifaa kuteseka kwa ajili ya Mungu, lakini leo wanafikiri kwamba ni aibu na hawakosi malalamiko. Hii ni kazi ya Shetani; inaonyesha kwamba mwanadamu amemilikiwa na Shetani. Ukikabiliwa na hali hii ni sharti uombe, na uibadilishe haraka uwezavyo—hii itakulinda dhidi ya mashambulizi ya Shetani. Ni wakati wa usafishaji mkali ambapo mwanadamu anaweza kujipata chini ya ushawishi wa Shetani kwa urahisi zaidi—kwa hivyo ni jinsi gani unapaswa kumpenda Mungu wakati wa usafishaji kama huu? Unapaswa kuyaita mapenzi yako, kuuweka moyo wako mbele ya Mungu na kutenga muda wako wa mwisho Kwake. Haijalishi jinsi gani Mungu hukusafisha, unafaa kuwa na uwezo wa kutia ukweli katika vitendo kutimiza mapenzi ya Mungu, na unafaa kujitolea kumtafuta Mungu na kutafuta mawasiliano. Nyakati kama hizi, zaidi unavyokaa tu, ndivyo utakuwa mtu hasi zaidi, na ndivyo itakuwa rahisi zaidi kwako kurudi nyuma. Wakati ambapo inakulazimu kutenda kazi yako, ingawa huitendi vyema, unafanya kila unachoweza, na unaifanya kwa kutumia tu upendo wako wa Mungu; bila kujali kile ambacho wengine husema—ikiwa wanasema umetenda vyema, au kwamba umetenda vibaya—motisha zako ni sahihi, na wewe sio wa kujidai, kwani unatenda kwa niaba ya Mungu. Wengine wanapokuelewa vibaya, unaweza kumwomba Mungu na kusema: “Ee Mungu! Siombi kwamba wengine wanivumilie au kunitendea vyema, wala kwamba wanielewe au kunikubali. Naomba tu kwamba niweze kukupenda moyoni mwangu, kwamba niwe na utulivu moyoni mwangu, na kwamba dhamiri yangu ni safi. Siombi kwamba wengine wanisifu, au kuniheshimu, ninatafuta tu kukuridhisha kutoka moyoni mwangu, ninatenda wajibu wangu kwa kufanya kila ninachoweza, na ingawa mimi ni mpumbavu na mjinga, na mwenye ubora wa tabia duni, na kipofu, najua kwamba Unapendeza, na niko tayari kukutolea kila ninacho.” Punde tu unapoomba kwa jinsi hii, upendo wako kwa Mungu huibuka, na unahisi utulivu zaidi moyoni mwako. Hili ndilo linalomaanishwa na kutenda upendo wa Mungu. Unavyopata uzoefu, utashindwa mara mbili na kufaulu mara moja, au pia ushindwe mara tano na kufaulu mara mbili, na unavyopata uzoefu kwa jinsi hii, ni katikati ya kushindwa tu ndipo utaweza kuona uzuri wa Mungu na kugundua kinachokosa ndani yako. Unapopitia hali kama hizi tena, unafaa kujitahadharisha, kutuliza mwendo wako, na kuomba mara nyingi zaidi. Polepole utakuza uwezo wa kushinda katika hali

kama hizi. Hilo linapofanyika, maombi yako yamekuwa yenye matokeo yanayotarajiwa. Unapooona umefanikiwa wakati huu, utafurahishwa ndani yako, na unapoomba utaweza kumhisi Mungu, na kuhisi kwamba uwepo wa Roho Mtakatifu haujakutoka—na ni hapo tu ndipo utajua jinsi Mungu hufanya kazi ndani yako. Kutenda kwa njia hii kutakupa njia inayoelekea katika uzoefu. Usipoutia ukweli katika vitendo, basi utakuwa bila uwepo wa Roho Mtakatifu ndani yako. Lakini ukiutia ukweli katika vitendo unapokumbana na mambo jinsi yalivyo, basi, ingawa unaumia ndani, Roho Mtakatifu atakuwa nawe baadaye, utaweza kuhisi uwepo wa Mungu unapoomba, utakuwa na nguvu ya kutenda maneno ya Mungu, na wakati wa mawasiliano na ndugu zako, hakutakuwa na chochote kinachosumbua dhamiri yako, na utahisi amani, na kwa jinsi hii, utaweza kufunua yale ambayo umefanya. Bila kujali yale ambayo wengine husema, utaweza kuwa na uhusiano wa kawaida na Mungu, hutazuiliwa na wengine, hutashindwa na lolote—na katika hili, utaonyesha kwamba kutenda kwako maneno ya Mungu kumekuwa kwa matokeo yanayotarajiwa.

Kadiri usafishaji wa Mungu ulivyo mkubwa, ndivyo mioyo ya watu inaweza kumpenda Mungu zaidi. Mateso ndani ya mioyo yao ni ya manufaa kwa maisha yao, wanaweza zaidi kuwa na amani mbele ya Mungu, uhusiano wao na Mungu ni wa karibu zaidi, na wanaweza kuona vizuri zaidi upendo wa juu kabisa wa Mungu na wokovu Wake wa juu kabisa. Petro alipitia usafishaji mamia ya mara, na Ayubu alipitia majaribio kadhaa. Ikiwa mngempenda kufanywa kamili na Mungu, nyinyi pia sharti mpitie usafishaji mamia ya mara; ni ikiwa tu mtapitia mchakato huu, na mtegemee hatua hii, ndiyo mnaweza kuridhisha mapenzi ya Mungu, na kufanywa kamili na Mungu. Usafishaji ndio njia bora zaidi ambayo Mungu hutumia kuwafanya watu kamili; usafishaji na majaribio makali pekee ndiyo yanaweza kusababisha kuonekana upendo wa kweli kwa Mungu ndani ya mioyo ya watu. Bila taabu, watu hukosa upendo wa kweli kwa Mungu; ikiwa hawajaribiwi ndani, na hawapitii usafishaji kwa kweli, basi mioyo yao daima itakuwa ikielea kwa nje. Baada ya kusafishwa hadi kiwango fulani, utayaona mapungufu na matatizo yako mwenyewe, utaona kiasi ambacho unakosa na kwamba huwezi kuzishinda zile shida nyingi unazokabiliwa nazo, na utaona jinsi kutotii kwako kulivyo kukubwa. Ni katika majaribu pekee ndipo watu wataweza kujua kwa kweli hali zao halisi, na majaribu huwafanya watu waweze kufanywa kamili vyema.

Katika maisha yake, Petro alipitia usafishaji mamia ya mara na alipitia majaribu mengi ya uchungu. Usafishaji huu ukawa msingi wa upendo wake mkubwa kabisa kwa Mungu na ukawa uzoefu muhimu zaidi katika maisha yake yote. Kwamba aliweza kuwa na upendo mkubwa kabisa wa Mungu ilikuwa, kwa namna moja, kwa sababu ya uamuzi wake kumpenda Mungu; la muhimu zaidi, hata hivyo, ilikuwa kwa sababu ya usafishaji na mateso aliyopitia. Mateso haya yakawa mwongozo wake katika njia ya kumpenda Mungu, na yakawa jambo lililokumbukwa

zaidi kwake. Ikiwa watu hawapitii uchungu wa usafishaji wanapompenda Mungu, basi upendo wao umejaa uchafu na mapendeleo yao wenyewe; upendo kama huu umejaa mawazo ya Shetani, na hauwezi hata kabisa kuridhisha mapenzi ya Mungu. Kuwa na azimio la kumpenda Mungu sio sawa na kumpenda Mungu kwa kweli. Hata ingawa yote wanayofikiria mioyoni mwao ni kwa ajili ya kumpenda Mungu, na kumridhisha Mungu, kana kwamba fikira zao hazina mawazo yoyote ya kibinadamu, kana kwamba zote ni kwa ajili ya Mungu, fikira zao zinapoletwa mbele ya Mungu, fikira kama hizi hazisifiwi wala kubarikiwa na Mungu. Hata wakati watu wameelewa kikamilifu ukweli wote—wakati wamekuja kuujua wote—hili haliwezi kusemwa kuwa ishara ya kumpenda Mungu, haiwezi kusemwa kwamba watu hawa hakika wanampenda Mungu. Licha ya kuelewa ukweli mwingi bila kupitia usafishaji, watu hawana uwezo wa kutia ukweli huu katika vitendo; ni wakati wa usafishaji tu ndipo watu wanaweza kuelewa maana halisi ya ukweli huu, hapo tu ndipo watu wanaweza kufahamu kwa kweli maana yao ya ndani. Wakati huo, wanapojaribu tena, wanaweza kutia ukweli katika vitendo kwa njia ya kufaa, na kulingana na mapenzi ya Mungu; wakati huo, mawazo yao ya kibinadamu yanapunguzwa, upotovu wao wa kibinadamu unapunguzwa, na hisia zao za kibinadamu zinapunguzwa; ni wakati huo tu ndipo utendaji wao ni onyesho la ukweli la upendo wa Mungu. Athari ya ukweli wa upendo wa Mungu haitimizwi kupitia ufahamu wa kusemwa au kuwa tayari kiakili, wala haiwezi kutimizwa kwa kueleweka tu. Inahitaji kwamba watu walipe gharama, na kwamba wapitie uchungu mwingi wakati wa usafishaji, na hapo tu ndipo upendo wao utakuwa safi, na wa kuupendeza moyo wa Mungu. Katika hitaji Lake kwamba mwanadamu ampende, Mungu hadai kwamba mwanadamu ampende kwa kutumia mapenzi makali, au mapenzi yake mwenyewe; kwa uaminifu tu na utumiaji wa ukweli kumtumikia ndipo mwanadamu anaweza kumpenda kwa kweli. Lakini mwanadamu huishi katikati ya upotovu, na hivyo hana uwezo wa kutumia ukweli na uaminifu kumtumikia Mungu. Yeye ama ni mwenye kutekwa na hisia kali kumhusu Mungu au hana hisia zozote na hajali; anampenda Mungu kwa kiwango cha juu zaidi au anamchukia kabisa. Wale ambao huishi katikati ya upotovu daima huishi katikati ya vipeo hivi viwili, daima wakiishi kwa kufuata mapenzi yao wenyewe lakini wakiadini kwamba wako sahihi. Ingawa Nimetaja hili mara kwa mara, watu hawana uwezo wa kulichukulia kwa uzito, hawawezi kuelewa kabisa umuhimu wake, na hivyo wanaishi katikati ya imani ya kujidanganya, katika madanganyo ya upendo kwa Mungu unaotegemea mapenzi yao wenyewe. Kotekote katika historia, kadiri mwanadamu ameendelea na enzi zimepita, mahitaji ya Mungu kwa mwanadamu yamekuwa ya juu zaidi, na Amezidi kudai kwamba mwanadamu awe kamili Kwake. Ilhali ufahamu wa mwanadamu kuhusu Mungu umekuwa usio yakini na wa dhahania zaidi na zaidi, na upendo wake wa Mungu kwa kufuatana umekuwa mchafu zaidi na zaidi. Hali ya mwanadamu na yote afanyayo yanazidi kubishana na mapenzi ya Mungu, kwa maana mwanadamu amepotoshwa kwa kina zaidi na Shetani. Hili linahitaji kwamba Mungu afanye kazi zaidi, na kazi kubwa zaidi, ya

wokovu. Mwanadamu anazidi kulipisha kwa nguvu katika mahitaji yake kwa Mungu, na upendo wake wa Mungu unapunguka zaidi na zaidi. Watu wanaishi katika uasi, bila ukweli, na wanaishi maisha yasiyo na ubinadamu; hawana tu upendo hata kidogo kwa Mungu, lakini pia wamejaa tele uasi na upinzani. Ingawa wanafikiri kuwa tayari wana upendo mkubwa kabisa kwa Mungu, na hawawezi kuwa wa hisani zaidi Kwake, Mungu haamini hivyo. Ni dhahiri kabisa Kwake jinsi upendo wa mwanadamu Kwake umeoza, na Hawajawahi kubadilisha maoni Yake ya mwanadamu kwa sababu ya ushawishi wa mwanadamu, wala kuwahi kulipiza ukarimu wa mwanadamu kwa sababu ya kujitolea kwake. Tofauti na binadamu, Mungu anaweza kutofautisha: Anajua yule anayempenda kwa kweli na yule asiyempenda, na badala ya kujawa na ari na kupotea kwa sababu ya mvuto wa ghafla wa mwanadamu, Anamtendea mwanadamu kulingana na asili na tabia ya mwanadamu. Mungu, hata hivyo, ni Mungu, na Ana hadhi Yake na utambuzi Wake; mwanadamu, hata hivyo, ni mwanadamu na Mungu hatapumbazwa na upendo wa mwanadamu ambao unazozana na ukweli. Kinyume chake, Anachukulia yote ambayo mwanadamu hufanya kwa jinsi ifaayo.

Anapokabiliwa na hali ya mwanadamu na mtazamo wake kwa Mungu, Mungu amefanya kazi mpya, Akimruhusu mwanadamu kuwa na ufahamu Wake na utiifu Kwake, na upendo pia na ushahidi. Hivyo, mwanadamu lazima apitie usafishaji wa Mungu kwake, na pia hukumu, ushughulikiaji na upogoaji Wake kwake, ambazo pasi nazo mwanadamu hangewahi kumjua Mungu, na hangewahi kuwa na uwezo wa kumpenda kwa kweli na kuwa na ushuhuda Kwake. Usafishaji wa Mungu kwa mwanadamu sio tu kwa ajili ya athari inayoegemea upande mmoja, bali kwa ajili ya athari inayogusia pande nyingi. Ni kwa jinsi hii tu ndiyo Mungu hufanya kazi ya usafishaji kwa wale ambao wako tayari kutafuta ukweli, ili upendo na uamuzi wao ufanywe timilifu na Mungu. Kwa wale walio tayari kuutafuta ukweli na wanaomtamani Mungu, hakuna kilicho cha maana zaidi, au cha usaidizi zaidi, kuliko usafishaji kama huu. Tabia ya Mungu haijulikani wala kueleweka kwa urahisi sana na mwanadamu, kwani Mungu, hatimaye, ni Mungu. Mwishowe, haiwezekani kwa Mungu kuwa na tabia sawa na mwanadamu, na hivyo si rahisi kwa mwanadamu kujua tabia Yake. Ukweli haumilikiwi kwa asili na mwanadamu, na hauleweki kwa urahisi na wale ambao wamepotoshwa na Shetani; mwanadamu hana ukweli na hana azimio la kutia ukweli katika vitendo, na asipoteseke, na asisafishwe au kuhukumiwa, basi uamuzi wake hautawahi kufanywa timilifu. Kwa watu wote, usafishaji ni wa kutesa sana na ni mgumu sana kukubali—ilhali ni katika usafishaji ndipo Mungu huweka wazi tabia Yake ya haki kwa mwanadamu, na Huweka hadharani mahitaji Yake kwa mwanadamu, na Hutoa nuru zaidi, na upogoaji na ushughulikiaji halisi zaidi; kwa kulinganisha mambo ya hakika na ukweli, Yeye humpa mwanadamu ufahamu mkubwa zaidi kujihusu na ukweli, na Humpa mwanadamu ufahamu mkubwa zaidi wa mapenzi ya Mungu, hivyo kumruhusu mwanadamu kuwa na upendo

wa kweli zaidi na safi zaidi wa Mungu. Haya ndiyo malengo ya Mungu katika kutekeleza usafishaji. Kazi yote Afanyayo Mungu kwa mwanadamu ina malengo yake na maana yake; Mungu hafanyi kazi isiyo na maana, wala Hafanyi kazi isiyo na manufaa kwa mwanadamu. Usafishaji haumaanishi kuondoa watu kutoka mbele ya Mungu, wala haumaanishi kuwaangamiza katika kuzimu. Unamaanisha kubadilisha tabia ya mwanadamu wakati wa usafishaji, kubadilisha motisha zake, mitazamo yake ya kale, kubadilisha upendo wake kwa Mungu, na kubadilisha maisha yake yote. Usafishaji ni jaribio la kweli la mwanadamu, na aina ya mafunzo halisi na ni wakati wa usafishaji tu ndipo upendo wake unaweza kutimiza wajibu wake wa asili.

Wanaompenda Mungu Wataishi Milele Katika Mwangaza Wake

Kiini cha imani ya watu wengi katika Mungu ni imani za kidini: Hawana uwezo wa kumpenda Mungu na wanaweza kumfuata Mungu tu kama roboti, bila kuweza kumtamani Mungu, ama kumwabudu. Wanamfuata tu kimyakimya. Watu wengi wanamwamini Mungu, lakini wapo wachache sana ambao humpenda Mungu; “wanamheshimu” tu Mungu kwa sababu wanaogopa majanga, au hata wanamstahi Mungu kwa sababu ni Mwenye nguvu na aliye juu—lakini katika kumheshimu na kuvutiwa kwao hakuna upendo au kutamani kwa kweli. Katika matukio wanayoyapitia wanataka chembe za ukweli, au hata miujiza fulani isiyokuwa na maana. Watu wengi hufuata tu, wanapitia njia mbaya ili tu kupokea baraka; hawataki ukweli, wala kumtii Mungu kwa kweli ili kupokea baraka za Mungu. Maisha ya imani kwa Mungu ya watu wote hayana maana, hayana thamani, na katika imani yao mna fikira na kazi zao za kibinafsi; hawaamini katika Mungu ili kumpenda Mungu, lakini kwa ajili ya kutaka kubarikiwa. Watu wengi hutenda jinsi wapendavyo, hufanya wanachokitaka, na kutojali anachopenda Mungu, au kama wanachokifanya ni kulingana na mapenzi ya Mungu. Watu kama hao hawawezi kupata imani ya kweli, sembuse upendo wa Mungu. Kiini cha Mungu sio tu kwa mwanadamu kuamini; vilevile ni, kwa mwanadamu kupenda. Lakini wengi wa wale wanaomwamini Mungu hawana uwezo wa kugundua hii “siri.” Watu hawathubutu kumpenda Mungu, wala hawajaribu kumpenda Yeye. Hawajawahi kugundua kuwa kuna mengi sana ya kupendeza kuhusu Mungu, hawajawahi kugundua kwamba Mungu ni Mungu anayempenda mwanadamu, na kwamba ni Mungu ambaye mwanadamu anapaswa kumpenda. Upendo wa Mungu umeonyeshwa katika kazi Yake: ni baada tu ya kupitia kazi Yake ndipo wanaweza wakagundua upendo Wake, ni katika matukio wanayopitia ya hakika tu ambapo wanaweza kufahamu upendo wa Mungu, na bila kuupitia katika maisha halisi, hakuna anayeweza kugundua kupendeza kwa Mungu. Kuna mengi ya kupendeza kumhusu Mungu, lakini bila ya kujihusisha na Yeye kwa hakika watu wengi

hawana uwezo wa kuyagundua. Hivi ni kusema, kama Mungu asingefanyika mwili, watu wasingekuwa na uwezo wa kujihusisha na Yeye, na kama wasingekuwa na uwezo wa kujihusisha na Yeye, pia wasingeweza kupitia Kazi Yake—na kwa hivyo upendo wao kwa Mungu ungetiwa doa la uongo mwingi na mawazo. Upendo wa Mungu ulio mbinguni si halisi kama upendo wa Mungu ulio ulimwenguni, kwa kuwa ufahamu wa watu kuhusu Mungu aliye mbinguni umejengwa katika mawazo yao, bali si kwa yale ambayo wameyaona kwa macho yao, na yale ambayo wameyapitia wao wenyewe. Mungu anapokuja ulimwenguni, watu wanaweza kuyaona matendo Yake halisi na upendo wake, na wanaweza kuona kila kitu katika matendo na tabia Zake za kawaida, ambayo ni mara elfu halisi kuliko ufahamu wa Mungu aliye mbinguni. Bila kujali ni vipi ambavyo watu wanampenda Mungu aliye mbinguni, hakuna kitu halisi kuhusu huu upendo, na umejaa mawazo ya kibinadamu. Haijalishi udogo wa upendo wao kwa Mungu aliye duniani, huu upendo ni halisi; hata kama ni kidogo, ungali ni halisi. Mungu huwafanya watu kumjua kupitia kazi halisi, na kupitia ufahamu huu Anapata upendo wao. Ni kama Petro: kama hangeishi na Yesu, haingewezekana yeye kumwabudu Yesu. Aidha, huu uaminifu ulijengwa kwenye uhusiano wake na Yesu. Ili kumfanya mwanadamu ampende, Mungu amekuja miongoni mwa wanadamu na kuishi na wanadamu, na yote Anayomfanya mwanadamu kuona na kupitia ni uhalisi wa Mungu.

Mungu hutumia uhalisi na ujio wa ukweli kuwafanya watu kuwa wakamilifu; maneno ya Mungu hutimiza sehemu ya kuwafanya watu kuwa wakamilifu, na hii ni kazi ya uelekezaji na kufungua njia. Hivi ni kusema, katika maneno ya Mungu lazima utafute njia ya matendo, na lazima utafute ufahamu wa maono. Kwa kuyaelewa haya mambo, mwanadamu atakuwa na njia na maono anapotenda, na kuweza kupata nuru kupitia maneno ya Mungu, ataweza kuelewa kuwa haya mambo hutoka kwa Mungu, na kuweza kutambua mengi. Baada ya kuelewa, lazima aingie katika uhalisia mara moja, na kutumia maneno ya Mungu kumridhisha Mungu katika maisha yake halisi. Mungu atakuelekeza katika mambo yote, na Atakupa njia ya matendo, na kukufanya uhisi kuwa Mungu anapendeza sana, na kukufanya uone kuwa kila hatua ya kazi ya Mungu ndani yako ni kwa ajili ya kukufanya uwe mkamilifu. Ukitaka kuona upendo wa Mungu, ukitaka kwa kweli kupitia katika upendo wa Mungu, hivyo ni lazima uzame katika uhalisi, ni lazima uzame katika maisha halisi, na kuona kwamba kila kitu afanyacho Mungu ni upendo, na wokovu, na kwamba watu waweze kuacha kile ambacho si safi, na kwa ajili ya kusafisha mambo ndani yao ambayo hayana uwezo wa kuridhisha mapenzi ya Mungu. Mungu hutumia maneno kumkimu mwanadamu na wakati huo huo kutengeneza mazingira katika maisha halisi ambayo huwaruhusu watu kupitia, na kama watu watakula na kunywa maneno mengi ya Mungu, basi wanapoyaweka katika vitendo, wanaweza kutatua matatizo yote katika maisha yao kwa kutumia maneno mengi ya Mungu. Hivi ni kusema, lazima uwe na maneno ya Mungu ili kuzama katika

uhalisi; kama huli na hunywi maneno ya Mungu, na huna kazi ya Mungu, basi hutakuwa na njia katika maisha halisi. Kama hujawahi kushiriki maneno ya Mungu, basi utashangaa wakati mambo yatakapokutokea. Unajua tu kwamba unapaswa kumpenda Mungu, lakini huwezi kutofautisha chochote, na huna njia ya vitendo; umevurugika na kuchanganyikiwa, na mara nyingine unaamini kuwa kwa kuuridhisha mwili unamridhisha Mungu—yote ambayo ni matokeo ya kutokula na kunywa maneno ya Mungu. Hivi ni kusema, kama huna usaidizi wa maneno ya Mungu, na kutapatapa tu katika uhalisi, basi kimsingi huna uwezo wa kupata njia ya vitendo. Watu kama hawa hawaelewi maana ya kumwamini Mungu, au hata kuelewa kumpenda Mungu kunamaanisha nini. Ikiwa, kwa kutumia nuru na uelekezaji wa maneno ya Mungu, unaomba mara kwa mara, na kuchunguza, na kutafuta, ambayo kwayo unagundua kile unachofaa kuweka katika vitendo, kutafuta fursa ya Kazi ya Roho Mtakatifu, unashirikiana na Mungu kwa kweli, na huvurugiki na kuchanganyikiwa, basi utakuwa na njia katika maisha halisi, na kumridhisha Mungu kwa kweli. Ukimridhisha Mungu, ndani yako kutakuwa na uelekezaji wa Mungu, na hasa kubarikiwa na Mungu, ambako kutakupa hisia za furaha: utahisi hasa umeheshimika kwa kuwa umemridhisha Mungu, na utahisi umeng'aa kwa ndani, na katika moyo wako utakuwa wazi na mwenye amani, dhamiri yako itafarijiwa na haitakuwa na shutuma, utahisi furaha ndani yako uwaonapo ndugu na dada zako. Hii ndio maana ya kufurahia upendo wa Mungu, na kwa kweli huku ndiko kumfurahia Mungu. Furaha ya watu kutokana na upendo wa Mungu inapatikana kwa kupitia matukio: kwa kupitia matatizo, na kupitia uwekaji ukweli katika vitendo, wanapata baraka za Mungu. Kama unasema tu Mungu anakupenda, kuwa Mungu amelipa gharama kubwa kwa watu, kuwa Mungu ameongea maneno mengi kwa uvumilivu na huruma, na Huokoa watu kila mara, utamkaji wako wa maneno haya ni upande mmoja tu wa kumfurahia Mungu. Ilhali, raha kubwa zaidi—kufurahia halisi—kungekuwa ni kwa watu kuweka ukweli katika vitendo katika maisha yako halisi, ambapo baadaye watakuwa na amani na kuwa wazi moyoni mwao, watahisi wakiwa wamesisimka, ndani yao, na kuwa Mungu anapendeza sana. Utaahisi kuwa gharama uliyoilipa inafaa sana. Baada ya kulipa gharama kubwa katika juhudi zako, utang'aa hasa ndani yako: utahisi kuwa unafurahia upendo wa Mungu kwa kweli, na kuelewa kuwa Mungu amefanya Kazi ya kuwaokoa watu, kuwa kuwasafisha watu ni kwa ajili ya kuwatakasu, na kuwa Mungu anawajaribu watu ili kupima kama wanampenda kwa kweli. Kama utaweka ukweli katika vitendo kwa njia hii, basi hatua kwa hatua utakuza ufahamu wazi zaidi wa kazi ya Mungu, na wakati huo utakuwa unahisi kuwa maneno ya Mungu mbele yako yatakuwa wazi kabisa. Kama unaweza kuelewa waziwazi ukweli mwingi, utahisi kuwa maswala yote ni rahisi kuweka katika vitendo, kuwa utashinda swala hili, na kushinda jaribio hilo, na utaona kuwa hakuna chochote kigumu kwako, ambacho kitakufanya kuwa mtu huru na aliyekombolewa. Kufikia hapa utakuwa ukifurahia upendo wa Mungu, na upendo wa Mungu wa kweli utakuwa umekushukia. Mungu hubariki wale ambao wana maono, ambao wana ukweli,

ambao wana ufahamu, na ambao wanampenda kwa kweli. Watu wakitaka kuuona upendo wa Mungu, lazima waweke ukweli katika vitendo katika maisha halisi, lazima wawe tayari kuvumilia mateso na kuacha hicho wanachokipenda na kumridhisha Mungu, mbali na machozi kwenye macho yao, lazima waweze kuuridhisha moyo wa Mungu. Kwa njia hii, kwa hakika Mungu atakubariki, na ukivumilia matatizo kama haya, yatafuatiwa na kazi ya Roho Mtakatifu. Kupitia kwa maisha halisi, na kutokana na kupitia maneno ya Mungu, watu wanaweza kuona upendo wa Mungu, na wanaweza kumpenda Mungu kwa ukweli ikiwa tu wameuonja upendo wa Mungu.

Kadiri unavyoweka ukweli katika vitendo, ndivyo unavyokuwa na ukweli; kadiri unavyoweka ukweli katika vitendo, ndivyo unavyokuwa na upendo wa Mungu; na kadiri unavyoweka ukweli katika vitendo, ndivyo unavyobarikiwa na Mungu. Kama utatenda kwa njia hii kila mara, upendo wa Mungu kwako utakuwezesha kuona polepole, jinsi tu ambavyo Petro alivyokuja kumjua Mungu: Petro alisema kuwa si kuwa Mungu ana busara ya kuumba mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo pekee, lakini, aidha, kuwa Ana busara ya kufanya kazi halisi ndani ya watu. Petro alisema kuwa Mungu hastahili tu upendo wa watu kwa sababu ya uumbaji Wake wa mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo, lakini, vilevile, kwa sababu ya uwezo Wake wa kuumba mwanadamu, kumwoko, kumfanya mwanadamu awe mkamilifu, na kutoa upendo wake kwa mwanadamu. Petro alimwambia Yesu: “Je, Hustahili upendo wa watu zaidi ya kuumba mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo? Kuna mengi ndani Yako ambayo yanapendeka, unatenda na kuendelea katika maisha halisi, Roho Wako ananigusa ndani, unanifundisha nidhamu, unanikemea—haya mambo yanastahili zaidi upendo wa watu.” Kama unataka kuona na kupitia upendo wa Mungu, basi lazima uzuru na kutafuta katika maisha halisi, na uwe tayari kuweka kando mwili wako. Lazima ufanye azimio hili: kuwa mtu mwenye uamuzi, ambaye anaweza kumridhisha Mungu katika mambo yote, bila ya kuzembea, au kutamani kuufurahisha mwili, kutoishi kwa ajili ya mwili lakini kuishi kwa ajili ya Mungu. Kunaweza kuwa na nyakati ambazo hukumridhisha Mungu. Hii ni kwa sababu huelewi mapenzi ya Mungu; wakati ujao, hata kama itahitaji juhudi zaidi, lazima umridhishe Mungu, na lazima usiuridhishe mwili. Unapopitia kwa njia hii, utakuja kumjua Mungu. Utaona kuwa Mungu angeweza kuumba mbingu na dunia na vitu vyote vilivyomo, na Amekuwa mwili ili watu wamwone kwa uhakika, na kujihusisha na Yeye, kuwa ana uwezo wa kuishi miongoni mwa wanadamu, kuwa Roho Wake aweza kufanya watu kuwa wakamilifu katika maisha halisi, kuwawezesha kuona upendo na uzoefu wa nidhamu Yake, kurudi Kwake, na baraka Zake. Kama huwa unapitia kwa njia hii, katika maisha halisi hutatenganishwa na Mungu, na kama siku moja uhusiano wako na Mungu utaacha kuwa wa kawaida, utaweza kupatwa na aibu, na kuweza kuhisi huzuni. Unapokuwa na uhusiano wa kawaida na Mungu, hutatamani kamwe kutaka

kumuacha, na siku moja Mungu akisema Atakuacha, utaogopa, na kusema kuwa ni heri ufe kuliko kuachwa na Mungu. Punde tu unapokuwa na hisia hizi, utahisi kuwa hakuna uwezo wa kumwacha Mungu, na kwa njia hii utakuwa na msingi, na utafurahia upendo wa Mungu wa kweli.

Mara nyingi watu husema kuwa wamemfanya Mungu kuwa maisha yao, lakini bado wanalipitia kupitia hatua hii. Wanasema tu kuwa Mungu ndiye maisha yao, kuwa Anawaongoza kila siku, kuwa wanakula na kunywa maneno Yake kila siku, na kuwa wanamwomba kila siku, na hivyo Amekuwa ndiye maisha yao. Ufahamu wa wanaosema hili ni wa juu juu. Ndani ya watu wengi hakuna msingi; maneno ya Mungu yamepandwa ndani yao, lakini bado hayajaota, au hata kuzaa tunda lolote. Hadi leo, umepitia uzoefu wa kiwango gani? Ni saa hii, baada ya Mungu kukulazimisha kuja umbali huu, ndio unahisi kuwa huwezi kumuacha Mungu. Siku moja ukishakuwa na uzoefu hadi kiwango fulani, Mungu akitaka kukuacha, hutaweza kufanya hivyo. Daima utahisi kuwa huwezi kuishi bila Mungu ndani yako; waweza kuwa bila mume, mke, au watoto, bila familia, bila mama au baba, bila kufurahia kwa mwili, lakini huwezi kuishi bila Mungu. Kuwa bila Mungu itakuwa kama kupoteza uhai wako, hutaweza kuishi bila Mungu. Unapopitia hadi kiwango hiki, utakuwa umefanikisha imani yako kwa Mungu, na kwa njia hii Mungu atakuwa maisha yako, atakuwa msingi wa kuishi kwako, na hutaweza tena kumuacha Mungu. Unapokuwa umepitia hadi kiwango hiki, utakuwa umefurahia upendo wa Mungu kwelikweli, uhusiano wako na Mungu utakuwa wa karibu mno, Mungu atakuwa maisha yako, upendo wako, na wakati huo utaomba kwa Mungu na kusema: “Ee Mungu! Siwezi kukuacha, wewe ndiye maisha yangu, naweza kuishi bila vitu vingine vyote—lakini bila Wewe siwezi kuendelea kuishi.” Hiki ni kimo halisi cha watu; ni maisha halisi. Watu wengine wamelazimika kufika walipo siku ya leo: lazima waendeleo wapende wasipende, na daima huhisi kuwa wako katika hali ngumu. Lazima ugundue kuwa Mungu yupo maishani mwako, kiasi kwamba kama Mungu angeondolewa kutoka katika moyo wako ingekuwa kama kupoteza uhai wako; Mungu lazima awe maisha yako, na lazima uwe huwezi kumwacha. Kwa njia hii utakuwa umekutana na Mungu, na kwa wakati huu, unapompenda Mungu, utampenda Mungu kwa kweli, na utakuwa upendo wa kipekee, upendo safi. Siku moja, matukio unayopitia yatakapokuwa kwamba maisha yako yamefikia kiwango fulani, unapomwomba Mungu, na kula na kunywa maneno ya Mungu, hutaweza kumwacha Mungu ndani, wala hutaweza kumsahau hata kama unataka. Mungu atakuwa maisha yako, waweza kuusahau ulimwengu, waweza kumsahau mkeo, mmeo, au watoto, lakini itakuwa vigumu kumsahau Mungu—hilo haliwezekani, haya ndiyo maisha yako halisi, na upendo wako wa ukweli kwa Mungu. Upendo wa watu kwa Mungu ufikiapo kiwango fulani, upendo wao kwa kitu kingine chochote huwezi kulinganishwa na upendo wao kwa Mungu; upendo wao kwa Mungu unapewa kipaumbele. Kwa njia hii wanaweza kuacha vitu

vingine vyote, na wawe tayari kukubali kushughulikiwa na kupogolewa na Mungu. Unapopata pendo kutoka kwa Mungu ambalo linazidi mengine yote, utaishi katika uhalisi, na katika upendo wa Mungu.

Punde tu Mungu anapokuwa uzima katika watu, wanakuwa hawana uwezo wa kumwacha Mungu. Je, hili sio tukio la Mungu? Hakuna ushuhuda mkubwa kuliko huu! Mungu amefanya kazi hadi kiwango fulani; Amewataka watu kutoa huduma, na kuadibiwa, au kufa, na watu hawajarudi nyuma, ambalo linaonyesha kuwa watu hawa wameshindwa na Mungu. Watu ambao wana ukweli ni wale ambao, katika matukio wanayopitia ya kweli, wanaweza kusimama imara katika ushuhuda wao, kusimama imara katika nafasi zao, kusimama katika upande wa Mungu, bila kurudi nyuma, na ambao wanaweza kuwa na uhusiano wa kawaida na watu wanaompenda Mungu, wale ambao, mambo yakishawatokea, wanaweza kumtii Mungu kabisa, na wanaweza kumtii Mungu hadi kifo. Matendo na ufunuo wako katika maisha halisi ndio ushuhuda wa Mungu, ni kuishi kwa kudhihirisha maisha ya mwanadamu na ushuhuda wa Mungu, na huku ni kufurahia upendo wa Mungu; unapopitia hadi kiwango hiki, matukio unayopitia yatakuwa yamekuwa na athari. Watu ambao wameuona upendo wa Mungu kwa kweli ni wale ambao wanaishi kwa kudhihirisha kwa kweli, ambao kila matendo yao yanapongezwa na wengine. Mavazi na kuonekana kwenu kwa nje hakupendezi, lakini wanaoishi kwa kudhihirisha maisha ya utiifu wa hali ya juu, ambao wanawasiliana kwa karibu maneno ya Mungu na huelekezwa na Mungu, na kupata nuru kutoka kwa Mungu, ambao huweza kuongea mapenzi ya Mungu katika maneno yao, na wanawasiliana kwa karibu uhalisi, ambao huelewa zaidi kuhusu kuhudumu katika Roho, wanaongea kwa wazi, ambao ni wenye heshima na kuaminika, ambao hawakabiliki na wana tabia nzuri, ambao wanaweza kutii mipango ya Mungu na kusimama imara katika ushuhuda wakati mambo yanapowatokea, ambao wana utulivu bila kujali wanachokumbana nacho. Watu wengine wangali wachanga, lakini wanatenda kama mtu mzima; wamekomaa, wana ukweli, wanapendwa na wengine—na hawa ndio watu ambao wana ushuhuda, na ndio udhihirisho wa Mungu. Ni sawa na kusema, wanapopitia mambo na kufikia kiwango fulani, ndani yao watakuwa na ufahamu juu ya Mungu, tabia zao za ndani zitakuwa zimeimarika. Watu wengi hawaweki ukweli katika vitendo na wengi hawasimami imara kwa ushuhuda wao. Ndani ya watu kama hao hakuna upendo wa Mungu, au ushuhuda kwa Mungu, na hawa ndio watu ambao wanachukiwa sana na Mungu. Wanasoma maneno ya Mungu katika mikutano, lakini wanachoishi kwa kudhihirisha ni Shetani, na huku ni kumfedhehesha Mungu, kumkashifu Mungu na kumkufuru Mungu. Ndani ya watu kama hawa, hakuna dalili ya upendo wa Mungu, na hawana kazi ya Roho Mtakatifu hata kidogo. Kwa hivyo maneno na matendo ya watu yanamwakilisha shetani. Kama moyo wako uko na amani na Mungu kila wakati, na huwa uko makini kwa watu na vitu vinavyokuzunguka, na kinachoendelea katika mazingira yako, na

unafahamu mzigo wa Mungu, na kila mara una moyo unaomheshimu Mungu, basi Mungu atakupua nuru ndani yako. Kanisani kuna watu ambao ni “wasimamizi”, wanatazama makosa ya wengine, kisha kunakili na kuwa kama wao. Hawana uwezo wa kutofautisha, hawachukii dhambi, hawachukii au kughadhibishwa na vitu vya Shetani. Watu kama hao wamejawa na vitu vya Shetani, na hatimaye wataachwa na Mungu kabisa. Wale ambao wana maono kama msingi wao, na ambao huandama maendeleo, ni wale ambao mioyo yao daima inamheshimu Mungu, ambao ni wa wastani katika maneno na vitendo vyao, ambao wasingetaka kumpinga Mungu, kumkasirisha Mungu, au Kazi ya Mungu kwao isiwe na thamani, au shida walizozipitia ziwe bure, au yale yote ambayo wameweka katika vitendo yapite bure. Ni watu ambao wako tayari kutoa juhudi zaidi na upendo wa Mungu katika njia iliyo mbele.

Watu wakimwamini Mungu, na kupitia maneno ya Mungu, kwa moyo unaomheshimu Mungu, basi ndani ya watu hao kunaweza kuonekana wokovu wa Mungu, na upendo wa Mungu. Watu hawa wana uwezo wa kumshuhudia Mungu, wanaishi kwa kudhihirisha ukweli, na kile wanachokikiri ni kweli, kile Mungu Alichu, na tabia ya Mungu, na wanaishi Kati ya upendo wa Mungu na wameona upendo wa Mungu. Watu wakitaka kumpenda Mungu, lazima wauonje upendo wa Mungu, na kuuona upendo wa Mungu; hapo tu ndipo wanaweza kupata kuamshiwa moyo ndani yao ambao unampenda Mungu, moyo ambao uko tayari kutumia rasilmali kwa ajili ya Mungu kwa heshima. Mungu hawafanyi watu kumpenda kupitia maneno na sura, au kwa mawazo yao, na Hawalazimishi watu kumpenda. Badala yake, Anawafanya wampende kwa hiari yao, na huwafanya kuyaona mapenzi Yake katika kazi Yake na matamshi, ambapo baadaye wanakuwa na upendo wa Mungu. Ni kwa njia hii tu ndio watu wanaweza kuwa na ushuhuda kwa Mungu. Watu hawampendi Mungu kwa sababu wameombwa na wengine kufanya vile, wala si msukumo wa hisia wa muda mfupi. Wanampenda Mungu kwa sababu wameuona upendo wake, na wameona kuwa kuna mengi kumhusu ambayo yanastahili upendo wao, kwa sababu wameona wokovu wa Mungu, busara, na matendo ya ajabu—na kutokana na hayo, wanamsifu Mungu kwa kweli, na kumtamani kwa kweli, na wanaamshiwa msisimko ndani yao kwamba hawawezi kuishi bila kumpata Mungu. Sababu ya wale ambao humshuhudia Mungu wanaweza kumtolea ushuhuda wa kufana ni kwa kuwa ushuhuda wao umekitwa kwenye msingi wa ufahamu wa kweli pamoja na matamano ya kweli kwa Mungu, si kutokana na msukumo wa hisia, lakini kulingana na ufahamu wa Mungu na tabia Zake. Kwa sababu wamepata kumjua Mungu, wanahisi kwamba lazima wamshuhudie Mungu, na kuwafanya wale wote wamtamano Mungu wamjue Mungu, na kufahamu upendo wa Mungu, na uhalisi Wake. Sawa na mapenzi ya watu kwa Mungu, ushuhuda wao ni wa hiari, ni halisi, na una umuhimu halisi na thamani. Si baridi, au tupu na usiokuwa na maana. Sababu ya wale tu wanaompenda Mungu kweli kuwa na thamani na maana katika maisha yao, na kuamini katika Mungu tu, ni kwa sababu watu hawa wanaishi

katika mwangaza wa Mungu, na wanaweza kuishi kwa ajili ya kazi ya Mungu na usimamizi Wake; hawaishi gizani, bali wanaishi katika mwangaza; hawaishi maisha yasiokuwa na maana, ila wanaishi maisha ambayo yamebarikiwa na Mungu. Ni wale tu ambao wanampenda Mungu wanaweza kumshuhudia Mungu, ndio tu mashahidi wa Mungu, ndio tu wamebarikiwa na Mungu, na ndio tu wanaweza kupokea ahadi za Mungu. Wanaompenda Mungu ni wandani wa Mungu, ndio watu ambao wamependwa na Mungu, na wanaweza kufurahia baraka pamoja na Mungu. Ni watu hawa tu ambao wataishi milele, na ni wao tu wataishi milele katika utunzaji na ulinzi wa Mungu. Mungu yuko kwa ajili ya kupendwa na watu, na anastahili upendo wa watu wote, lakini si watu wote ambao wanaweza kumpenda Mungu, na si watu wote wanaweza kumshuhudia Mungu na kushiriki mamlaka pamoja na Mungu. Kwa sababu wanaweza kumshuhudia Mungu, na kutoa juhudi zao zote kwa kazi ya Mungu, wanaompenda Mungu kwa kweli wanaweza kutembea mahala popote chini ya mbingu bila ya mtu yeyote kujaribu kuwapinga, na wanaweza kushika mamlaka na kutawala watu wote wa Mungu. Hawa watu wanakusanyika pamoja kutoka pembe zote za dunia, wanazungumza lugha tofauti na ni wa rangi tofauti, lakini kuishi kwao kuna maana sawa, wote wana moyo unaompenda Mungu, wote wana ushuhuda sawa, na wana maazimio sawa, na mapenzi sawa. Wale ambao wanampenda Mungu wanaweza kutembea ulimwenguni kote wakiwa huru, wanaomshuhudia Mungu wanaweza kusafiri duniani kote. Watu hawa wamependwa wa Mungu, wamebarikiwa na Mungu, na wataishi milele katika mwangaza Wake.

Ni Wale Wanaolenga Kutenda tu Ndio Wanaoweza Kukamilishwa

Katika siku za mwisho, Mungu alipata mwili ili kufanya kazi Aliyopaswa kufanya na kutekeleza huduma Yake ya maneno. Alikuwa yeye mwenyewe ili kufanya kazi kati ya wanadamu kwa lengo la kuwakamilisha wale watu ambao wanaipendeza nafsi Yake. Kutoka wakati wa uumbaji hadi leo Yeye hufanya tu hiyo kazi wakati wa siku za mwisho. Ni wakati wa siku za mwisho tu ambapo Mungu alipata mwili ili kufanya kazi kwa kiwango kikubwa. Ingawa Yeye huvumilia shida ambazo watu wanaweza kupata ugumu kuvumilia, ingawa Yeye kama Mungu mkuu ana unyenyekevu wa kuwa mtu wa kawaida, hakuna kipengele cha kazi Yake kimecheleweshwa, na mpango Wake haujatupwa katika mchafuko hata kidogo. Anafanya kazi kulingana na mpango Wake wa awali. Mojawapo ya madhumuni ya kupata mwili huku ni kuwashinda watu. Mengine ni kuwakamilisha watu Anaowapenda. Yeye hutamani kuwaona kwa macho Yake mwenyewe watu Anaowakamilisha, na Yeye hutaka kujionea Mwenyewe jinsi watu Anaowakamilisha humshuhudia. Sio mtu mmoja ambaye hukamilishwa, na sio wawili. Hata hivyo, ni kikundi cha watu wachache sana. Kikundi hiki cha watu huja kutoka nchi mbalimbali

za dunia, na kutoka kwa makabila mbalimbali ya ulimwengu. Kusudi la kufanya kazi hii nyingi ni kukipata kikundi hiki cha watu, kupata ushuhuda ambao kikundi hiki cha watu humtolea, na kupata utukufu ambao Yeye hupata kupitia kwa kikundi hiki cha watu. Yeye hafanyi kazi ambayo haina umuhimu, wala hafanyi kazi ambayo haina thamani. Inaweza kusemwa kuwa, kwa kufanya kazi nyingi sana, lengo la Mungu ni kuwakamilisha watu wote ambao Yeye anataka kuwakamilisha. Katika wakati wowote wa ziada Alio nao nje ya hili, Atawaondosha wale walio waovu. Jua kwamba Haifanyi kazi hii kubwa kwa sababu ya wale walio waovu; kwa kinyume, Yeye hufanya kadri Awezavyo kwa sababu ya idadi hiyo ndogo ya watu ambao hawana budi kukamilishwa na Yeye. Kazi ambayo Yeye hufanya, maneno ambayo Yeye hunena, siri ambayo Yeye hufichua, na hukumu Yake na adhabu zote ni kwa ajili ya idadi hiyo ndogo ya watu. Yeye hakupata mwili kwa sababu ya wale walio waovu, sembuse wao kuchochea ghadhabu kubwa ndani Yake. Yeye husema ukweli, na huzungumzia kuingia, kwa sababu ya wale wataokamilishwa, Alipata mwili kwa sababu yao, na ni kwa sababu yao Yeye hutoa ahadi na baraka Zake. Ukweli, kuingia, na maisha katika ubinadamu ambayo Yeye huzungumzia si kwa ajili ya wale walio waovu. Yeye hutaka kuepuka kuzungumza na wale walio waovu, na hutaka kuwapa wale ambao watakamilishwa ukweli wote. Lakini kazi Yake inahitaji kwamba, kwa sasa, wale walio waovu waruhusiwe kufurahia baadhi ya utajiri Wake. Wale ambao hawatekelezi ukweli, ambao hawamridhishi Mungu, na ambao hukatiza kazi Yake wote ni waovu. Hawawezi kukamilishwa, na wanachukiwa kabisa na kukataliwa na Mungu. Kwa kinyume, watu ambao hutia ukweli katika vitendo na wanaweza kumridhisha Mungu na ambao hujitolea wenyewe kabisa katika kazi ya Mungu ndio watu ambao watakamilishwa na Mungu. Wale ambao Mungu hutaka kuwakamilisha sio wengine bali ni kikundi hiki cha watu, na kazi ambayo Mungu hufanya ni kwa ajili ya watu hawa. Ukweli ambao Yeye huzungumzia unaelekezwa kwa watu ambao wako tayari kuutia katika vitendo. Yeye huwa hazungumzi na watu ambao hawatii ukweli katika vitendo. Ongezeko la umaizi na ukuaji wa utambuzi ambao Yeye huzungumzia umelengwa kwa watu ambao wanaweza kutekeleza ukweli. Anapozungumza juu ya wale ambao watakamilishwa, ni watu hawa Anaozungumza kuwahusu. Kazi ya Roho Mtakatifu inaelekezwa kwa watu ambao wako tayari kutenda ukweli. Mambo kama kuwa na hekima na binadamu yanaelekezwa kwa watu ambao wako tayari kutia ukweli katika vitendo. Wale ambao hawatekelezi ukweli wanaweza kusikia maneno mengi, lakini kwa sababu wao ni waovu sana kiasili na hawavutiwi na ukweli, kile wanachoelewa is mafundisho ya dini na maneno tu, na nadharia tupu, bila kujali hata kidogo kuingia kwao katika maisha. Hakuna hata mmoja wao aliye mwaminifu kwa Mungu; wao wote ni watu wanaomwona Mungu lakini hawawezi kumpata; wote wamehukumiwa na Mungu.

Roho Mtakatifu ana njia ya kutembea katika kila mtu, na humpa kila mtu fursa za

kukamilishwa. Kupitia uhasi wako unajulishwa upotovu wako mwenyewe, na kisha kwa njia ya kuacha uhasi utapata njia ya kutenda, na huku ndiko kukamilishwa kwako. Aidha, kwa njia ya mwongozo na mwangaza wa siku zote wa mambo fulani chanya ndani yako, utatimiza shughuli yako kwa kuamili na kukua katika umaizi na kupata utambuzi. Wakati hali zako ni nzuri, uko tayari hasa kusoma neno la Mungu, na hasa tayari kumwomba Mungu, na unaweza kuyahusisha mahubiri unayoyasikia na hali zako mwenyewe. Kwa nyakati kama hizo Mungu hukupatia nuru na kukuangaza ndani, na kukufanya utambue mambo fulani ya kipengele chanya. Huku ni kukamilishwa kwako katika kipengele chanya. Katika hali hasi, wewe ni dhaifu na hasi, na huhisi kuwa huna Mungu moyoni mwako, lakini Mungu hukuangaza, akikusaidia kupata njia ya kutenda. Kutoka nje ya hili ni kupata ukamilisho katika hali chanya. Mungu anaweza kumkamilisha mwanadamu katika vipengele hasi na chanya. Inategemea kama unaweza kupata uzoefu, na kama wewe hufuatilia kukamilishwa na Mungu. Kama kwa hakika unatafuta kukamilishwa na Mungu, basi kilicho hasi hakiwezi kukufanya upoteze, lakini kinaweza kukuletea mambo ambayo ni halisi zaidi, na kinaweza kukufanya uweze zaidi kujua kile kilichopunguka ndani yako, uweze zaidi kufahamu sana hali zako halisi, na kuona kwamba mtu hana kitu, wala si kitu; kama hupitii majaribio, hujui, na daima utahisi kuwa wewe ni wa hadhi ya juu kuliko wengine na bora kuliko kila mtu mwingine. Kwa njia hii yote utaona kwamba yote yaliyotangulia yalifanywa na Mungu na kulindwa na Mungu. Kuingia katika majaribio hukuacha bila upendo au imani, huna sala, na huwezi kuimba nyimbo—na, bila kulitambua, katikati ya hili unakuja kujijua. Mungu ana njia nyingi za kumkamilisha mwanadamu. Yeye hutumia mazingira ya kila aina ili shughulikia tabia potovu ya mwanadamu, na hutumia vitu mbalimbali ili kumuweka mwanadamu wazi; katika suala moja Yeye humshughulikia mwanadamu, katika jingine Yeye humuweka mwanadamu wazi, na katika jingine Yeye humfichua mwanadamu, kuzichimbua na kuzifichua “siri” katika vina vya moyo wa mwanadamu, na kumwonyesha mwanadamu asili yake kwa kuzifichua hali zake nyingi. Mungu humkamilisha mwanadamu kupitia mbinu nyingi—kupitia ufunuo, ushughulikiaji, usafishwaji, na kuadibu—ili mwanadamu aweze kujua kwamba Mungu ni wa vitendo.

Ni nini mnachokitaka sasa? Kukamilishwa na Mungu, kumjua Mungu, kumpata Mungu—ama labda mnataka kujiendeza kama Petro wa miaka ya 90, ama kuwa na imani kubwa zaidi kuliko ile ya Ayubu, ama labda mnataka kuitwa wenye haki na Mungu na kufika mbele ya kiti cha Mungu cha enzi, ama kuweza kumridhisha Mungu duniani na kumtolea ushuhuda wa nguvu na mkubwa. Bila kujali kile mnachotaka, kwa jumla mnataka kwa ajili ya kuokolewa na Mungu. Bila kujali iwapo unataka kuwa mtu mwenye haki ama unataka namna ya Petro, ama imani ya Ayubu, ama kukamilishwa na Mungu, yote ni kazi ambayo Mungu anamfanyia mwanadamu. Hivyo ni kusema, bila kujali unachokitafuta, yote ni kwa ajili ya kukamilishwa na Mungu, yote

ni kwa ajili ya kupitia neno la Mungu, ili kuuridhisha moyo wa Mungu; yote ni kwa ajili ya kugundua uzuri wa Mungu, yote ni kwa ajili ya kutafuta njia ya kutenda katika uzoefu halisi kwa lengo la kuweza kuiacha tabia yako ya uasi, kufanikisha hali ya kawaida ndani yako mwenyewe, kuweza kufuata kabisa mapenzi ya Mungu, kuwa mtu sahihi, na kuwa na nia sahihi katika kila kitu unachokifanya. Sababu ya wewe kupitia vitu hivi vyote ni kufikia kumjua Mungu na kufanikisha ukuaji wa maisha. Ingawa kile unachokipitia ni neno la Mungu, na kile unachokipitia ni matukio halisi, watu, mambo, na vitu katika mazingira yako, hatimaye unaweza kumjua Mungu na kukamilishwa na Mungu. Kutafuta kitembea njia ya mtu mwenye haki au kutafuta kutia neno la Mungu katika vitendo, hizi ndizo njia. Kumjua Mungu na kukamilishwa na Mungu ndiyo hatima. Kama unatafuta sasa kukamilishwa na Mungu, au kumshuhudia Mungu, kwa ujumla, hatimaye ni ili kumjua Mungu; ni ili kwamba kazi Anayoifanya ndani yako sio ya bure, ili hatimaye uje kuujua uhalisi wa Mungu, kujua ukuu Wake, vivyo hivyo hata zaidi kuujua unyenyekevu wa Mungu na hali Yake ya kutoonekana, na kujua kazi nyingi ambazo Mungu hufanya ndani yako. Mungu amejinyenyekeza Mwenyewe kwa kiwango fulani, kufanya kazi Yake katika watu hawa wachafu na wapotovu, na kukikamilisha kikundi hiki cha watu. Mungu hakupata mwili tu ili kuishi na kula kati ya watu, kuwalisha watu, kutoa wanachohitaji watu. Jambo muhimu zaidi ni kwamba Yeye hufanya kazi Yake kubwa ya wokovu na ushindi kwa watu hawa walio na upotovu usiovumilika. Alikuwa katika kiini cha joka kubwa jekundu ili kuwaokoa watu hawa wapotovu mno, ili watu wote waweze kubadilishwa na kufanywa wapya. Tatizo kubwa ambalo Mungu huvumilia siyo tu shida ambayo Mungu mwenye mwili huvumilia, lakini hasa ni kwamba Roho wa Mungu hupitia udhalilishaji uliokithiri—Yeye hujinyenyekeza na kujificha Mwenyewe sana kiasi kwamba Yeye huwa mtu wa kawaida. Mungu alipata mwili na kuchukua mfano wa mwili ili watu waone kwamba Ana maisha ya kawaida ya binadamu, na kwamba ana mahitaji ya kawaida ya binadamu. Hili linatosha kuthibitisha kwamba Mungu amejinyenyekeza Mwenyewe kwa kiwango fulani. Roho wa Mungu hufanyika katika mwili. Roho Wake ni wa juu sana na mkuu, lakini Yeye huchukua mfano wa mwanadamu wa kawaida, wa mwanadamu asiye muhimu ili kufanya kazi ya Roho Wake. Ubora wa tabia, umaizi, hisi, ubinadamu, na maisha ya kila mmoja wenu vinaonyesha kwamba hamfai kweli kupokea kazi ya Mungu ya aina hii. Hakika hamfai kumruhusu Mungu kuvumilia shida kama hiyo kwa ajili yenu. Mungu ni mkubwa sana. Yeye ni mkuu sana, na watu ni duni sana na wa hali ya chini, lakini Yeye bado huwafanyia kazi. Yeye hakupata mwili tu ili kuwaruzuku watu, kuzungumza na watu, Yeye hata huishi pamoja na watu. Mungu ni mnyenyekevu sana, wa hupendeka sana. Ikiwa punde upendo wa Mungu unapotajwa, mara tu neema ya Mungu inapotajwa, unatoa machozi unapotamka sifa kubwa, ukifika katika hali hii, basi una maarifa ya kweli ya Mungu.

Kuna mchepuko katika kutafuta kwa watu siku hizi; wao hutafuta tu kumpenda Mungu na

kumridhisha Mungu, lakini hawana maarifa yoyote juu ya Mungu, na wametelekeza nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu ndani yao. Hawana maarifa ya kweli ya Mungu kama msingi. Kwa njia hii wanapoteza nguvu wakati uzoefu wao unapoendelea. Wale wote wanaotafuta kuwa na maarifa ya kweli ya Mungu, ingawa hapo zamani hawakuwa katika hali nzuri, na walielekea kwa uhasi na udhaifu, na mara nyingi walitoa machozi, wakakata tamaa, na kupoteza tumaini—sasa, wakati wanapopata uzoefu zaidi, hali zao zinaimarika. Baada ya kushughulikiwa na kuvunjwa, na baada ya kupitia mfululizo mmoja wa majaribu na usafishaji, walikuwa na maendeleo makubwa. Hizo hali hasi zinapunguka, na kumekuwa na mabadiliko kiasi katika tabia zao za maisha. Huku wakipitia majaribu zaidi, mioyo yao inaanza kumpenda Mungu. Kuna kanuni kwa kukamilishwa kwa watu na Mungu, ambayo ni kwamba Yeye hukupa nuru kwa kutumia sehemu yako inayofaa ili uwe na njia ya kutenda na unaweza kujitenga na hali zote hasi, ikisaidia roho yako kupata uhuru, na ikikufanya uweze kumpenda zaidi. Kwa njia hii, unaweza kuiacha tabia potovu ya Shetani. Wewe huna hila na uko wazi, ukiwa tayari kujijua nakutia ukweli katika vitendo. Mungu hakika atakubariki, kwa hiyo unapokuwa dhaifu na hasi, Yeye hukupa nuru maradufu, Akikusaidia kujijua zaidi, kuwa tayari kujitubia, na kuweza zaidi kutenda mambo ambayo unapaswa kuyatenda. Ni kwa njia hii tu ambapo moyo wako unahisi amani na utulivu. Mtu ambaye kwa kawaida huzingatia kumjua Mungu, ambaye huzingatia kujijua, ambaye huzingatia vitendo vyake mwenyewe ataweza kupokea kazi ya Mungu mara kwa mara, mara kwa mara kupokea mwongozo na nuru kutoka kwa Mungu. Hata ingawa yuko katika hali hasi, anaweza kugeuka mara moja, iwe ni kwa sababu ya matendo ya dhamiri au kwa sababu ya nuru kutoka kwa neno la Mungu. Mabadiliko ya tabia ya mtu hufanikishwa daima anapojua hali yake mwenyewe halisi na kujua tabia na kazi ya Mungu. Mtu ambaye yuko tayari kujijua na yuko tayari kuwasiliana ataweza kutekeleza ukweli. Aina hii ya mtu ni mtu ambaye ni mwaminifu kwa Mungu, na mtu ambaye ni mwaminifu kwa Mungu ana ufahamu wa Mungu, uwe ni wa kina au wa juu juu, haba au maridhawa. Hii ni haki ya Mungu, na ni kitu ambacho watu hupata, ni faida yao wenyewe. Mtu ambaye ana maarifa ya Mungu ni yule ambaye ana msingi, ambaye ana maono. Mtu wa aina hii ana hakika kuhusu mwili wa Mungu, na ana hakika kuhusu neno la Mungu na kazi ya Mungu. Bila kujali jinsi Mungu hufanya kazi au kuzungumza, au jinsi watu wengine husababisha vurugu, anaweza kushikilia msimamo wake, na kuwa shahidi kwa Mungu. Kadiri mtu alivyo katika njia hii ndivyo anavyoweza kutekeleza zaidi ukweli anaouelewa. Kwa sababu daima anatenda neno la Mungu, yeye hupata ufahamu zaidi wa Mungu, na analo azimio la kuwa shahidi kwa Mungu milele.

Kuwa na utambuzi, kuwa na utii, na kuwa na uwezo wa kubaini mambo ili uwe hodari katika roho ina maana kuwa maneno ya Mungu yanakuangaza na kukupa nuru ndani mara tu unapokabiliwa na kitu fulani. Huku ni kuwa hodari katika roho. Kila kitu ambacho Mungu

hufanya ni kwa ajili ya kusaidia kufufua roho za watu. Kwa nini Mungu daima husema kuwa watu ni wa kujijali na wajinga? Ni kwa sababu roho za watu zimekufa, na wamekuwa wa kutojali kiasi kwamba hawajui kabisa mambo ya roho. Kazi ya Mungu ni kuyafanya maisha ya watu yaendeleo na ni kusaidia roho za watu zichangamke, ili waweze kubaini mambo ya roho, na wao daima waweze kumpenda Mungu mioyoni mwao na kumridhisha Mungu. Ufikaji mahali hapa huonyesha kwamba roho ya mtu imefufuliwa, na wakati mwingine atakapokabiliwa na kitu fulani, anaweza kuonyesha hisia mara moja. Yeye huitikia mahubiri, na kuonyesha hisia haraka kwa hali mbalimbali. Huku ndiko kufanikisha uhodari wa roho. Kuna watu wengi ambao wana majibu ya haraka kwa tukio la nje, lakini mara tu kuingia katika uhalisi au mambo kinaganaga ya roho yanapotajwa, wao huwa wa kutojali na wajinga. Wao huelewa kitu tu kikiwa ni dhahiri. Hizi zote ni ishara za kuwa wa kutojali kiroho na mjinga, za kuwa na uzoefu kidogo wa mambo ya roho. Watu wengine ni hodari wa roho na wana utambuzi. Mara tu wanaposikia maneno yanayoonyesha hali zao, wanaharakisha kuyaandika. Mara wanaposikia maneno kuhusu kanuni za kutenda, wanaweza kuyakubali na kuyatumia katika uzoefu wao unaofuata. Huyu ni mtu ambaye ni hodari katika roho. Kwa nini anaweza kuonyesha hisia haraka hivyo? Ni kwa sababu yeye hulenga mambo haya katika maisha ya kila siku. Anaposoma maneno ya Mungu, anaweza kuzipima hali zake kwa kuyatumia na kujitafakari. Anaposikia ushirika na mahubiri na kusikia maneno yanayoleta nuru na mwanga, anaweza kuyapokea mara moja. Ni sawa na kumpa mtu mwenye njaa chakula; anaweza kula mara moja. Ukimpa chakula mtu asiye na njaa, hana haraka kuonyesha hisia. Daima wewe humwomba Mungu, na kisha unaweza kuonyesha hisia mara moja unapokabiliwa na kitu fulani: kile Mungu huhitaji katika jambo hili, na jinsi unavyopaswa kutenda. Mungu alikuongoza juu ya suala hili mara ya mwisho; unapokabiliwa na kitu cha aina hii leo, kwa kawaida utajua jinsi ya kutenda kwa namna inayoridhisha moyo wa Mungu. Ikiwa unatenda daima kwa njia hii na daima upate uzoefu kwa njia hii, wakati fulani utakuwa stadi kwayo. Wakati unasoma neno la Mungu unajua ni mtu wa aina gani Mungu anamzungumzia, unajua ni aina gani ya hali za roho anayozungumzia, na unaweza kuelewa jambo muhimu na kulitia katika vitendo; hii inaonyesha kuwa unaweza kupata uzoefu. Kwa nini watu wengine hawana jambo hili? Ni kwa sababu hawaweki jitihada nyingi katika kipengele cha kutenda. Ingawa wako tayari kutia ukweli katika vitendo, hawana umaizi wa kweli katika utondoti wa huduma, katika utondoti wa ukweli katika maisha yao. Wanachanganyikiwa jambo linapotokea. Kwa njia hii, unaweza kupotoshwa nabii wa uongo au mtume wa uongo anapokuja. Lazima ushiriki mara nyingi kuhusu maneno na kazi ya Mungu—ni kwa njia hii tu ndiyo utaweza kuelewa ukweli na kukuz utambuzi. Ikiwa huelewi ukweli, basi hutakuwa na utambuzi. Kwa mfano, kile Mungu husema, jinsi Mungu hufanya kazi, yale yaliyo matakwa Yake kwa watu, ni watu wa namna gani unapaswa kuwasiliana nao, na ni watu wa aina gani unaopaswa kuwakataa—ni lazima ushiriki mara nyingi kuhusu mambo haya. Ukipitia neno la Mungu kwa

njia hii daima, utaelewa ukweli na uelewe vizuri vitu vingi, na utakuwa na utambuzi pia. Ni nini kufundishwa nidhamu na Roho Mtakatifu, ni nini lawama inayotokana na nia ya mwanadamu, ni nini mwongozo kutoka kwa Roho Mtakatifu, ni nini mpango wa mazingira, ni nini maneno ya Mungu yanatolea nuru ndani, kama huna uhakika juu ya mambo haya, hutakuwa na utambuzi. Unapaswa kujua kile ambacho huja kutoka kwa Roho Mtakatifu, ni nini tabia ya uasi, jinsi ya kulitii neno la Mungu, na jinsi ya kuacha uasi wako mwenyewe; ikiwa una ufahamu wa vitendo wa mambo haya, utakuwa na msingi; kitu kinapotendeka, utakuwa na ukweli unaofaa wa kutumia kukipima na maono yanayofaa kama msingi. Utakuwa na kanuni katika kila kitu unachofanya, na utaweza kutenda kulingana na ukweli. Halafu maisha yako yatajazwa na nuru ya Mungu, yatajazwa na baraka za Mungu. Mungu hatamtendea vibaya mtu yeyote ambaye humtafuta kwa kweli. Hatamtendea vibaya mtu yeyote ambaye huishi kwa kumdhihirisha na ambaye hushuhudia kwa ajili Yake, na hatamlaani mtu yeyote ambaye kwa kweli anaweza kuona kiu ya ukweli. Ikiwa, unapokula na kunywa maneno ya Mungu, unaweza kuzingatia hali yako mwenyewe ya kweli, kuzingatia vitendo vyako mwenyewe, na kuzingatia ufahamu wako mwenyewe, basi, unapokabiliwa na tatizo, utapokea nuru na utapata ufahamu wa utendaji. Kisha utakuwa na njia ya kutenda na utakuwa na utambuzi kwa kila kitu. Mtu aliye na ukweli si rahisi kudanganywa, na rahisi kutenda kwa vurugu au kutenda kwa kupita kiasi. Kwa sababu ya ukweli amelindwa, na pia kwa sababu ya ukweli yeye hupata ufahamu zaidi. Kwa sababu ya ukweli ana njia zaidi za kutenda, hupata fursa zaidi za Roho Mtakatifu kufanya kazi ndani yake, na hupata fursa zaidi za kukamilishwa.

Kazi ya Roho Mtakatifu na Kazi ya Shetani

Unaelewa vipi umaalum katika roho? Roho Mtakatifu hufanya vipi kazi ndani ya mwanadamu? Shetani hufanya vipi kazi ndani ya mwanadamu? Roho waovu hufanya vipi kazi ndani ya mwanadamu? Na maonyesho ya kazi hii ni yapi? Wakati kitu kinakufanyikia, je, kinakuja kutoka kwa Roho Mtakatifu, na je, unapaswa kukiheshimu, au kukikataa? Utendaji halisi wa watu huibua mengi ambayo ni ya mapenzi ya kibinadamu ilhali ambayo watu daima huamini kutoka kwa Roho Mtakatifu. Mengine hutoka kwa roho waovu, ilhali watu bado hudhani yanatoka kwa Roho Mtakatifu, na wakati mwingine Roho Mtakatifu huwaongoza watu kutoka ndani, ilhali watu wanaogopa kwamba mwongozo kama huo hutoka kwa Shetani, na hawathubutu kutii, wakati kwa kweli ni nuru ya Roho Mtakatifu. Hivyo, bila utofautishaji hakuna njia ya kupitia wakati uzoefu kama huo kwa hakika unakufanyikia, na bila utofautishaji, hakuna njia ya kupata maisha. Roho Mtakatifu hufanya kazi vipi? Roho waovu hufanya kazi vipi? Nini hutoka kwa mapenzi ya mwanadamu? Na ni nini hutoka kwa mwongozo na nuru ya Roho Mtakatifu? Kama unaelewa amri za kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya mwanadamu, basi utaweza kukuza maarifa yako na kutofautisha katika maisha yako ya kila siku na wakati wa

uzoefu wako halisi; utakuja kumjua Mungu, utaweza kumwelewa na kumtambua Shetani, hutachanganyikiwa katika kutii ama kufuatilia kwako, na utakuwa mtu ambaye fikira zake zi wazi, na ambaye hutii kazi ya Roho Mtakatifu.

Kazi ya Roho Mtakatifu ni aina ya mwongozo wa kimatendo na kupata nuru kwa hali nzuri. Haiwaruhusu watu kuwa baridi. Huwaletea faraja, huwapa imani na uamuzi na kuwawezesha kufuatilia kufanywa kamili na Mungu. Wakati Roho Mtakatifu hufanya kazi, watu wanaweza kuingia kwa vitendo; wao si baridi wala hawalazimishwi, lakini ni wa kimatendo. Wakati Roho Mtakatifu hufanya kazi, watu wana faraja na wenye radhi, na wako tayari kutii, na wana furaha kujinyenyekeza, na hata ingawa wana maumivu na ni dhaifu ndani, wana uamuzi wa kushirikiana, wanateseka kwa furaha, wanaweza kutii, na hawajatiwa doa na mapenzi ya mwanadamu, hawajatiwa doa na fikira ya mwanadamu, na hakika hawajatiwa doa na tamaa na motisha za mwanadamu. Wakati watu wanapitia kazi ya Roho Mtakatifu, ndani yao ni watakatifu hasa. Wale ambao wanamiliki kazi ya Roho Mtakatifu huishi kwa kudhihirisha upendo wa Mungu, upendo wa kaka na dada zao, na kufurahia vitu ambavyo Mungu hufurahia na kuchukia vitu ambavyo Mungu huchukia. Watu ambao wanaguswa na kazi ya Roho Mtakatifu wana ubinadamu wa kawaida, na wao daima hufuatilia ukweli na wanamiliki ubinadamu. Wakati Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani ya watu, hali zao huwa nzuri zaidi na zaidi, na ubinadamu wao unakuwa wa kawaida zaidi na zaidi, na ingawa ushirikiano wao mwingine unaweza kuwa mpumbavu, motisha zao ziko sahihi, kuingia kwao ni kwa hali nzuri, hawajaribu kukatiza, na hakuna nia mbaya ndani yao. Kazi ya Roho Mtakatifu ni ya kawaida na ya kweli, Roho Mtakatifu hufanya kazi kwa mwanadamu kulingana na amri za maisha ya kawaida ya mwanadamu, na Yeye huwapa nuru na kuongoza watu kulingana na ufuatiliaji halisi wa watu wa kawaida. Wakati Roho Mtakatifu hufanya kazi kwa watu, Yeye huwaongoza na kuwapa nuru kulingana na mahitaji ya watu wa kawaida, Anawakimu kwa msingi wa mahitaji yao, na Yeye huwaongoza na kuwapa nuru kwa hali nzuri kwa msingi wa kile ambacho wanakosa, na kwa upungufu wao. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kuwapa watu nuru na kuwaongoza katika maisha halisi; wakipitia maneno ya Mungu katika maisha yao tu ndipo wanaweza kuona kazi ya Roho Mtakatifu. Iwapo, katika maisha yao ya kila siku, watu wako katika hali nzuri na wana maisha ya kawaida ya kiroho, basi wanamiliki kazi ya Roho Mtakatifu. Katika hali kama hiyo, wakati wanakula na kunywa maneno ya Mungu wana imani, wakati wanaomba wanatiwa moyo, wakati kitu kinawafanyikia wao si baridi, na wakati kinawafanyikia wanaweza kuona masomo ambayo Mungu anawahitaji kujifunza, na hawako baridi, ama dhaifu, na ingawa wana ugumu wa kweli, wako tayari kukubali mipango yote ya Mungu.

Ni matokeo yapi yanayotimizwa na kazi ya Roho Mtakatifu? Unaweza kuwa mpumbavu, na kunaweza kuwa hakuna utofautishaji wowote ndani yako, lakini Roho Mtakatifu anapaswa tu

kufanya kazi ili kuwe na imani ndani yako, ili wewe daima uhisi kwamba huwezi kumpenda Mungu vya kutosha, ili uwe tayari kushiriki, uwe tayari kushiriki bila kujali ugumu mkuu ulio mbele. Mambo yatakufanyikia na haitakuwa wazi kwako iwapo yanatoka kwa Mungu ama kwa Shetani, lakini utaweza kungoja, na hutakuwa baridi wala mzembe. Hii ndiyo kazi ya kawaida ya Roho Mtakatifu. Wakati Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani yao, watu bado hukabiliwa na ugumu wa kweli, wakati mwingine wanalia, na wakati mwingine kuna mambo ambayo hawawezi kuyashinda, lakini hii yote ni hatua ya kazi ya kawaida ya Roho Mtakatifu. Ingawa hawashindi mambo hayo, na ingawa, wakati huo, wao ni dhaifu na hulalamika, baadaye bado wanaweza kumpenda Mungu na imani dhabiti. Ubaridi wao hauwezi kuwazuia kuwa na uzoefu wa kawaida, na bila kujali kile watu wengine husema, na jinsi wanavyowashambulia, bado wanaweza kumpenda Mungu. Wakati wa maombi, daima wanahisi kwamba walikuwa wadeni wa Mungu sana, na wanaamua kumridhisha Mungu na kuukataa mwili wakati wanakabiliwa na mambo kama hayo tena. Nguvu hii inaonyesha kuna kazi ya Roho Mtakatifu ndani yao, na hii ndiyo hali ya kawaida ya kazi ya Roho Mtakatifu.

Ni kazi ipi hutoka kwa Shetani? Katika kazi inayotoka kwa Shetani, maono ndani ya watu si yakini na ni dhahania, na hawana ubinadamu wa kawaida, motisha za vitendo vyao si sahihi, na ingawa wanataka kumpenda Mungu, daima kuna lawama ndani yao, na lawama hizi na fikira daima zinaingilia ndani yao, zikizuia kukua kwa maisha yao, na kuwasitisha kuja mbele ya Mungu katika hali ya kawaida. Hii ni kusema, punde tu kazi ya Shetani inapokuwa ndani ya watu, mioyo yao haiwezi kuwa kwa amani mbele ya Mungu, na hawajui cha kufanya, kuona mkutano kunawafanya kutaka kuhepa, na hawawezi kufumba macho yao wakati wengine wanaomba. Kazi ya roho waovu huharibu uhusiano wa kawaida kati ya mwanadamu na Mungu, na huvuruga maono ya awali ya watu au njia yao ya awali ya kuingia katika maisha, katika mioyo yao hawawezi kamwe kumkaribia Mungu, daima mambo hufanyika ambayo huwasababishia vurugu na kuwatia pingu, na mioyo yao haiwezi kupata amani, kuacha upendo wao wa Mungu bila nguvu, na kuwafanya kusunoneka. Hayo ndiyo maonyesho ya kazi ya Shetani. Kazi ya Shetani inadhihirishwa katika yafuatayo: kutoweza kushikilia msimamo na kuwa na ushuhuda, kukusababisha kuwa mtu ambaye ana makosa mbele ya Mungu, na ambaye hana uaminifu kwa Mungu. Kwa kuingilia kwa Shetani, unapoteza upendo na uaminifu kwa Mungu ndani yako, unaondolewa uhusiano wa kawaida na Mungu, hufuatili ukweli, ama kujiendeleza, unarudi nyuma, na kuwa baridi, unajipendeza, unaachia uenezaji wa dhambi, na huchukii dhambi; zaidi ya hayo, kuingilia kwa Shetani kunakufanya mpotovu, kunasababisha mguso wa Mungu kutoweka ndani yako, na kunakufanya kulalamika kuhusu Mungu na kumpinga Yeye, kukufanya uwe na shaka na Mungu, na hata kuna hatari ya wewe kumwacha Mungu. Hii yote ni kazi ya Shetani.

Wakati kitu kinakufanyikia katika maisha yako ya kila siku, unapaswa kutofautishaje kati ya iwapo kinatoka kwa kazi ya Roho Mtakatifu ama kwa kazi ya Shetani? Wakati hali za watu ni za kawaida, maisha yao ya kiroho na maisha yao katika mwili ni ya kawaida, na mantiki yao ni ya kawaida na ya mpangilio; kwa jumla kile wanachokipitia na kuja kujua ndani yao wakati huu kinaweza kusemwa kutoka kwa kuguswa na Roho Mtakatifu (kuwa na umaizi au kumiliki maarifa ya juu juu wanapokula na kunywa maneno ya Mungu, au kuwa waaminifu wakati mambo yanawafanyikia, au kuwa na nguvu ya kumpenda Mungu wakati mambo yanafanyika—haya yote ni ya Roho Mtakatifu). Kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya mwanadamu hasa ni ya kawaida: mwanadamu hana uwezo wa kuihisi, na inaonekana kuwa ni kupitia kwa mwanadamu mwenyewe—lakini kwa kweli ni kazi ya Roho Mtakatifu. Katika maisha ya kila siku, Roho Mtakatifu hufanya kazi ndogo na kubwa kwa kila mtu, na ni tu kwamba kiwango cha kazi hii hubadilika. Watu wengine ni wa ubora mzuri wa tabia, wanaelewa mambo haraka, na nuru ya Roho Mtakatifu hasa ni kubwa ndani yao; watu wengine ni wa ubora duni wa tabia, na inachukua muda mrefu zaidi kwao kuelewa mambo, lakini Roho Mtakatifu huwagusa ndani, na wao, pia, wanaweza kutimiza uaminifu kwa Mungu—Roho Mtakatifu hufanya kazi kwa wale wote wanaomfuatilia Mungu. Wakati, katika maisha ya kila siku, watu hawampingi Mungu, au kuasi dhidi ya Mungu, hawafanyi mambo ambayo yanazozana na usimamizi wa Mungu, na hawakatizi kazi ya Mungu, ndani ya kila mmoja wao Roho wa Mungu hufanya kazi kwa kiwango kikubwa au kidogo, na kuwagusa, kuwapa nuru, kuwapa nguvu, na kuwasisimua kuingia kimatendo, sio kuwa wazembe au kutamani raha za mwili, kuwa tayari kutenda ukweli, na kutamani maneno ya Mungu—hii yote ni kazi ambayo hutoka kwa Roho Mtakatifu.

Wakati hali ya watu si ya kawaida, wanatelekezwa na Roho Mtakatifu, kuna malalamishi ndani yao, motisha zao si sahihi, wao ni wazembe, wanajiingiza katika tamaa za kimwili, na mioyo yao huasi dhidi ya ukweli, na haya yote hutoka kwa Shetani. Wakati hali za watu si za kawaida, wakati wana uovu ndani yao na wamepoteza mantiki yao ya kawaida, wametelekezwa na Roho Mtakatifu, na hawawezi kumhisi Mungu ndani yao, huu ndiyo wakati Shetani anafanya kazi ndani yao. Ikiwa watu daima wana nguvu ndani yao na daima humpenda Mungu, basi kwa jumla wakati mambo yanawafanyikia yanatoka kwa Roho Mtakatifu, na yeyote wanayekutana naye ni tokeo la mipango ya Mungu. Ambayo ni kusema, wakati hali zako ni za kawaida, wakati upo katika kazi kubwa ya Roho Mtakatifu, basi haiwezekani Shetani kukufanya uyumbayumbe; juu ya msingi huu inaweza kusemwa kwamba kila kitu hutoka kwa Roho Mtakatifu, na ingawa unaweza kuwa na mawazo yasiyo sahihi, unaweza kuyakataa, na usiyafuate. Hii yote hutoka kwa kazi ya Roho Mtakatifu. Shetani huingilia katika hali zipi? Wakati hali zako si za kawaida, wakati hujaguswa na Mungu, na uko bila kazi ya Mungu, na wewe ni mkavu na bure ndani, wakati unasali kwa Mungu lakini huelewi chochote, na kula na kunywa maneno ya Mungu lakini

hujapewa nuru au mwangaza—wakati kama huo ni rahisi kwa Shetani kufanya kazi ndani yako. Kwa maneno mengine, wakati umeachwa na Roho Mtakatifu na huwezi kumhisi Mungu, basi mambo mengi hukufanyikia ambayo hutoka kwa majaribu ya Shetani. Shetani hufanya kazi wakati sawa na ule Roho Mtakatifu hufanya kazi, na huingilia kwa mwanadamu wakati sawa na ule Roho Mtakatifu hugusa ndani ya mwanadamu; wakati kama huo, hata hivyo, kazi ya Roho Mtakatifu huchukua nafasi ya kwanza, na watu ambao hali zao ni za kawaida wanaweza kushinda, ambao ni ushindi wa kazi ya Roho Mtakatifu juu ya kazi ya Shetani. Wakati Roho Mtakatifu anafanya kazi, bado kuna tabia potovu ndani ya watu; hata hivyo, wakati wa kazi ya Roho Mtakatifu, ni rahisi kwa watu kugundua na kutambua uasi, malengo na ughushi wao. Ni hapo tu ndipo wanahisi majuto na wanakuwa tayari kutubu. Hivyo, uasi wao na tabia potovu zinaondolewa polepole ndani ya kazi ya Mungu. Kazi ya Roho Mtakatifu hasa ni ya kawaida, na Anapofanya kazi kwa watu bado wana shida, bado wanalia, bado wanateseka, bado ni dhaifu, na bado kuna mengi ambayo si dhahiri kwao, ilhali katika hali kama hiyo wanaweza kujisitisha kurudia mazoea mabaya, na wanaweza kumpenda Mungu, na ingawa wanalia na wana dhiki ndani, bado wanaweza kumsifu Mungu; kazi ya Roho Mtakatifu hasa ni ya kawaida, na si ya mwujiza hata kidogo. Watu wengi sana huamini kwamba, punde tu Roho Mtakatifu huanza kufanya kazi, mabadiliko hutokea katika hali ya watu na mambo muhimu kuwahusu yanaondolewa. Imani kama hizo ni za uwongo. Roho Mtakatifu afanyapo kazi ndani ya mwanadamu, mambo baridi ya mwanadamu bado yako hapo na kimo chake kinabaki sawa na awali, lakini ana mwangaza na nuru ya Roho Mtakatifu, na hivyo hali yake ni ya kimatendo zaidi, hali ndani yake ni za kawaida, na anabadilika kwa haraka. Katika uzoefu wa kweli wa watu, kimsingi wanapitia kazi ya Roho Mtakatifu au Shetani, na iwapo hawawezi kuwa na madaraka juu ya hali hizi, na hawatofautishi, basi uzoefu wa kweli hauwezekani, sembuse mabadiliko katika tabia. Hivyo, ufunguo wa kuwa na uzoefu wa kazi ya Mungu ni kuweza kubaini mambo kama haya; kwa njia hii, itakuwa rahisi zaidi kwao kupitia.

Kazi ya Roho Mtakatifu ni maendeleo mazuri, ilhali kazi ya Shetani ni kurudi nyuma kwa namna mbaya, uasi, kumpinga Mungu, kupoteza imani kwa Mungu, kutotaka hata kuimba nyimbo za kidini na kuwa dhaifu sana kiasi cha kutoweza kutimiza wajibu wa mtu. Kila kitu kitokacho kwa nuru ya Roho Mtakatifu ni cha kawaida sana; hakilazimishwi kwako. Ukikifuata, basi utakuwa na amani; usipokifuata, basi baadaye utakaripiwa. Ukiwa na nuru ya Roho Mtakatifu, basi hakuna ufanyacho kitakachoingiliwa au kuzuiliwa, utawekwa huru, kutakuwa na njia ya kutenda katika vitendo vyako, na hutapatwa na vizuizi vyovyote, na kuweza kutekeleza mapenzi ya Mungu. Kazi ya Shetani hucusababishia usumbufu katika mambo mengi; inakufanya kutotaka kusali, kuwa mzembe sana kula na kunywa maneno ya Mungu, na kutotaka kuishi maisha ya kanisa, na inakutenganisha na maisha ya kiroho. Kazi ya Roho Mtakatifu haiingili

maisha yako ya kila siku, na haiingilii maisha yako ya kawaida ya kiroho. Huwezi kutambua mambo mengi katika wakati ambapo yanatokea, lakini, baada ya siku chache, moyo wako unakuwa angavu na akili yako inakuwa safi. Unakuja kuwa na ufahamu juu ya mambo ya roho, na polepole unaweza kutambua ikiwa wazo limetoka kwa Mungu au kwa Shetani. Mambo mengine kwa dhahiri yanakufanya umpinge Mungu na kuasi Mungu, au kukusitisha kuyaweka maneno ya Mungu katika vitendo, na mambo haya yote hutoka kwa Shetani. Mambo mengine si dhahiri, na huwezi kujua ni nini wakati huo; baadaye, mnaweza kuona maonyesho yao, na kisha kufanya utambuzi. Kama mnaweza kutambua ni vitu vipi vinavyotoka kwa Shetani na ni vipi vinavyoelekezwa na Roho Mtakatifu, basi hamtapotoshwa kwa urahisi katika uzoefu wako. Wakati mwingine, hali zako zisipokuwa nzuri, una mawazo fulani yanayokutoa katika hali yako baridi—ambalo huonyesha kwamba wakati hali zako ni zisizofaa, mawazo yako mengine yanaweza pia kutoka kwa Roho Mtakatifu. Sio ukweli kwamba wakati wewe ni baridi, mawazo yako yote yanatumwa na Shetani; huo ungekuwa ukweli, basi ni lini ungeweza kugeukia hali ile nzuri? Baada ya kuwa baridi kwa kipindi cha muda, Roho Mtakatifu anakupa fursa kukamilishwa, Anakugusa, na kukutoa katika hali yako baridi.

Baada ya kujua kazi ya Roho Mtakatifu ni ipi, na kazi ya Shetani ni ipi, unaweza kulinganisha haya na hali yako mwenyewe wakati wa uzoefu wako, na uzoefu wako mwenyewe, na kwa njia hii kutakuwa na ukweli mwingi zaidi unaohusiana na kanuni katika uzoefu wako. Baada ya kuelewa mambo haya, utaweza kudhibiti hali yako halisi, utaweza kutofautisha kati ya watu na matukio, na hutahitajika kutumia nguvu nyingi sana katika kupata kazi ya Roho Mtakatifu. Bila shaka, hiyo ni ilimradi motisha zako ziko sahihi, na ilimradi uko tayari kutafuta, na kutenda. Lugha kama hii—lugha inayohusiana na kanuni—inapaswa kuonyeshwa katika uzoefu wako. Bila hiyo, uzoefu wako utakuwa umejaa kukatizwa na Shetani, na umejaa maarifa ya upuuzi. Ikiwa huelewi jinsi Roho Mtakatifu hufanya kazi, basi huelewi jinsi unapaswa kuingia, na ikiwa huelewi jinsi Shetani hufanya kazi, basi huelewi jinsi unapaswa kuwa mwangalifu katika nyayo zako. Watu wanapaswa kuelewa jinsi Roho Mtakatifu hufanya kazi na jinsi Shetani hufanya kazi; ni sehemu ya lazima ya uzoefu wa watu.

Onyo kwa Wale Wasiotenda Ukweli

Wale miongoni mwa ndugu ambao daima hueneza ubaya wao ni vibaraka wa Shetani, na hulivuruga kanisa. Watu hawa lazima siku moja wafukuzwe na kuondolewa. Katika imani yao kwa Mungu, ikiwa watu hawana moyo wa kumcha Mungu ndani yao, ikiwa hawana moyo ambao ni mtiifu kwa Mungu, basi sio tu kwamba hawatashindwa kufanya kazi yoyote ya Mungu, lakini kinyume na hayo watakuwa watu wanaovuruga kazi ya Mungu na wanaomwasi Mungu. Wakati ambapo mtu anayeamini Mungu hamtii Mungu ama kumcha Mungu lakini badala yake

anamwasi, basi hii ndiyo aibu kuu zaidi kwa muumini. Ikiwa usemi na mwenendo wa muumini daima havina mpango na bila kizuizi kama asiyeamini, basi huyu muumini ni mwovu zaidi kumpiku asiyeamini; yeye ni ibilisi halisi. Wale walio kanisani ambao wanaeneza matamshi yao yenye sumu, wale miongoni mwa ndugu ambao wanasambaza uvumi, kuchochea utangano na kufanya magenge wanapaswa kufukuzwa kutoka kanisani. Lakini watu hawa wamezuiwa kwa kuwa sasa ni enzi tofauti ya kazi ya Mungu, kwa sababu wamehukumiwa kuwa vyombo vya kuondolewa. Wale waliopotoshwa na Shetani wote wana tabia iliyopotoka. Hata hivyo, baadhi ya watu wana tabia potovu tu, huku kuna wengine walio tofauti: Si tu kwamba wana tabia potovu za kishetani, lakini asili zao pia ni mbovu kupita kiasi. Si tu kwamba maneno yao na vitendo vyao vinafichua tabia zao potovu za kishetani; watu hawa, aidha ndio Shetani wa kweli. Tabia yao inakatiza na kuvuruga kazi ya Mungu, inaharibu uingiaji wa kina ndugu katika uzima, na kuharibu maisha ya kawaida ya kanisa. Mbwa mwitu hawa waliovalia ngozi ya kondoo lazima waondolewe nje siku moja, na mtu lazima awe na mtazamo usiojizuia kwa vibaraka hawa wa Shetani; mtu lazima awe na mtazamo wa kuachwa kwao. Ni katika kufanya hili pekee ndipo mtu ataweza kusimama upande wa Mungu na wale wasioweza kufanya hili wako katika ushirika na Shetani. Mungu daima yumo mioyoni mwa wale wanaomwamini Mungu kwa kweli na daima wana moyo wa kumcha Mungu, moyo wa kumpenda Mungu. Wale wanaomwamini Mungu lazima wayafanye mambo kwa moyo wa uangalifu na wenye busara, na yote wanayoyafanya yanapasa kulingana na matakwa ya Mungu na yaweze kuuridhisha moyo wa Mungu. Hawapaswi kuwa wabishi, wakifanya watakavyo, hayo hayafai katika utaratibu mtakatifu. Watu hawawezi kuipunga bendera ya Mungu kwa madaha na kucharuka kila mahali, wakienda kwa mikogo na kutapeli kotekote; kutenda haya ni tendo la uasi la juu zaidi. Familia zina masharti zao na mataifa yana sheria zao; je, hali sio hivi hata zaidi katika nyumba ya Mungu? Je, matarajio sio makali hata zaidi? Je, hakuna amri nyingi hata zaidi za utawala? Watu wana uhuru wa kutenda watakayo, lakini amri za usimamizi za Mungu haziwezi kubadilishwa kwa hiari. Mungu ni Mungu asiyewaruhusu watu kumkosea; Yeye ni Mungu anayewaua watu. Je, watu kweli hawajui hili tayari?

Kila moja ya kanisa lina watu wanaolivuruga kanisa, watu wanaokatiza kazi ya Mungu. Watu hawa wote ni Shetani wanaojifanya katika familia ya Mungu. Watu kama hawa ni waigizaji wazuri: wanakuja mbele Yangu na uchaji mkubwa, wakiinama na kuchakura, wakiishi kama mbwa koko, wakijitolea “yote” waliyo nayo ili kufanikisha malengo yao wenyewe—lakini mbele ya kina ndugu, anaonyesha sura yake mbaya. Anapomwona mtu akiutenda ukweli anamshambulia na kumtenga; anapomwona mtu wa kutisha kumpiku yeye mwenyewe, anamsifu mno na kujipendekeza kwake, wakitenda kama viongozi wa kiimla kanisani. Inaweza kusemwa kuwa mengi ya makanisa yana aina hii ya “nyoka mwovu wa ndani,” aina hii ya “mbwa wa

kupakata” kati yao. Wanatembea kwa siri kwa pamoja, wakikonyezana na kuashiriana, na hakuna hata mmoja wao anayetenda ukweli. Yeyote aliye na sumu zaidi ndiye “ibilisi mkuu,” na yeyote aliye na hadhi ya juu zaidi huwaongoza, akipeperusha bendera yao juu zaidi. Watu hawa wanakuwa huru na kufanya wanachotaka kanisani, wakieneza ubaya wao, wakiachilia kifo, wakifanya watakavyo, wakisema wanachopenda, bila anayethubutu kuwakomesha, wakijawa na tabia za kishetani. Punde tu wanapoanza kusababisha usumbufu, hewa ya kifo inaingia ndani ya kanisa. Wale wanaotenda ukweli katika kanisa wanaachwa na wanashindwa kufikia uwezo wao, ilhali wale wanaovuruga kanisa na kusambaza kifo wanakuwa huru na kufanya wanachotaka kanisani. Cha ziada ni, watu wengi huwafuata. Aina hii ya kanisa iko chini ya udhibiti wa Shetani na ibilisi ni mfalme wao. Iwapo watu wa kanisa hawataamka na kuwafukuza hao ibilisi wakuu, basi pia watakuja kuangamia siku moja. Kuanzia leo na kuendelea hatua lazima zichukuliwe dhidi ya kanisa la aina hii. Ikiwa wale wanaoweza kutenda ukweli kidogo hawatafuti kufanya hivyo, basi kanisa hilo litaondolewa. Ikiwa hakuna mtu yeyote kanisani aliye radhi kuutenda ukweli, hakuna yeyote anayeweza kuwa shahidi kwa Mungu, basi kanisa hilo linapasa kutengwa kabisa, miunganisho yao na makanisa mengine kukatizwa. Hili linaitwa “kuzika kifo”; hii ndiyo maana ya kumfukuza Shetani. Iwapo kanisa lina waonevu kadhaa wa hapo, na wanafuatwa na “nzi wadogo” wasio na ufahamu kabisa, na ikiwa washiriki wa kanisa, hata baada ya kuona ukweli, bado hawawezi kukataa vifungo na kuchezeza na hawa waonevu—basi hawa wajinga wataondolewa mwishoni. Ingawa nzi hawa wadogo wanaweza kuwa hawajafanya lolote baya, wao ni wenye hila hata zaidi, wadanganyifu hata zaidi na wenye kukwepa hata zaidi na kila mtu aliye namna hii ataondolewa. Hakuna yeyote atakayeachwa! Wale walio wa Shetani watarudishwa kwa Shetani, ilhali wale walio wa Mungu hakika watakwenda kutafuta ukweli; hili linaamuliwa na asili zao. Acheni wale wote wanaomfuata Shetani waangamie! Hakuna huruma watakayoonyeshwa watu hawa. Acheni wale wanaofuata ukweli wapate utoaji na muwakubalie kufurahia neno la Mungu hadi mioyo yao itosheke. Mungu ni mwenye haki; Yeye hawatendei watu kwa udhalimu. Ikiwa wewe ni ibilisi basi hutakuwa na uwezo wa kuutenda ukweli. Ikiwa wewe ni mtu anayetafuta ukweli basi ni wazi kuwa hutatekwa nyara na Shetani—hili halina tashwishi yoyote.

Wale wasiotafuta kuendelea daima wanataka wengine wawe wabaya na watepetevu kama wao wenyewe, wale wasiotenda ukweli wanawaonea gere wale wanaotenda ukweli. Wale wasiotenda ukweli daima wanataka kuwadanganya wale wapumbavu na wasio na ufahamu. Mambo ambayo watu hawa wanaeneza yanaweza kukufanya usawijike, kuteleza kwenda chini, kuwa na hali isiyokuwa ya kawaida na kujawa na kiza ndani yako; yanaweza kukufanya usogezwe mbali na Mungu, na yanakufanya uuthamini mwili na kujihusisha na tamaa. Wale ambao hawapendi ukweli, ambao daima humshughulikia Mungu kwa uzembe hawana maarifa ya

binafsi, na tabia zao huwashawishi watu kufanya dhambi na kuasi Mungu. Hawaweki ukweli katika vitendo wala kuwaruhusu wengine kutenda ukweli. Wanathamini dhambi na hawana chuki kwao wenyewe. Hawajifahamu wenyewe na huwakomesha wengine kujifahamu wenyewe, na huwakomesha wengine kuwa na matamano ya kujua ukweli. Wale wanaowadanganya hawawezi kuona mwangaza na huanguka gizani, hawajijui wenyewe, na ukweli kwao si wazi na wanakuwa mbali zaidi na zaidi na Mungu. Hawaweki ukweli katika vitendo na huwakomesha wengine kutenda ukweli, wakiwaleta watu hao wajinga mbele yao. Badala ya kusema kuwa wanamwamini Mungu ingekuwa vyema kusema kuwa wanawaamini mababu zao, kwamba kile wanachoamini ni sanamu zilizo mioyoni mwao. Ingekuwa vyema kwa wale watu wanaosema kuwa wanamfuata Mungu kufungua macho yao watazame vizuri waone ni nani wanayemwamini hasa: Je, ni Mungu unayemwamini hakika, ama Shetani? Ikiwa unajua kuwa unayemwamini si Mungu ila sanamu zako mwenyewe, basi ni vyema kabisa usiseme kuwa wewe ni muumini. Ikiwa hakika hujui unayemwamini ni nani, basi, pia, ni vyema kabisa usiseme kuwa wewe ni muumini. Kusema hivi kutakuwa kukufuru! Hakuna anayekushurutisha umwamini Mungu. Msiseme kuwa mnaniamini Mimi, kwa kuwa Niliyasikia maneno hayo hapo kale wala Sitamani kuyasikia tena, kwa kuwa mnachoamini ni sanamu zilizo katika mioyo yenu na nyoka waovu wa ndani walio miongoni mwenu. Wale wanaotikisa vichwa vyao wanaposikia ukweli, wanaotabasamu sana wanaposikia mazungumzo ya kifo ni watoto wa Shetani, na wote ni vyombo vya kuondolewa. Kuna watu wengi kanisani ambao hawana ufahamu, na jambo la uongo linapotendeka wanasimama tu upande wa Shetani. Wanapoitwa vibaraka wa Shetani wanahisi kuwa wamekosewa sana. Wanasemekana kuwa hawana ufahamu, lakini daima wanasimama upande usiokuwa na ukweli. Hakujakuwa na wakati muhimu ambapo wamesimama upande wa ukweli, hakuna wakati mmoja ambapo hawasimami na kutetea mjadala juu ya ukweli. Je, kweli hawana ufahamu? Kwa nini daima wao husimama upande wa Shetani isipotarajiwa? Kwa nini hawasemi neno lolote la haki ama lenye mantiki kwa ukweli? Je, hali hii kweli imetokana na kuchanganyikiwa kwao kwa ghafla? Kadri mtu anapokuwa na ufahamu mdogo, ndivyo anavyozidi kushindwa kusimama upande wa ukweli. Je, hili linaonyesha nini? Je, halionyeshi kuwa wale wasio na ufahamu wanapenda uovu? Je, halionyeshi kuwa wale wasio na ufahamu ni watoto waaminifu wa Shetani? Je, ni kwa nini daima wanaweza kusimama upande wa Shetani na kuzungumza lugha moja naye? Kila neno na tendo lao, na maonyesho yao yanathibitisha vya kutosha kuwa wao sio wapenzi wa ukweli kwa namna yoyote, lakini badala yake wao ni watu wanaochukia ukweli. Kwamba wanaweza kusimama upande wa Shetani kunadhihirisha kuwa hakika Shetani anawapenda ibilisi hawa wadogo wanaopigana kwa ajili ya Shetani katika maisha yao yote. Je, taarifa hizi za kweli si wazi sana? Ikiwa hakika wewe ni mtu unayependa ukweli, basi kwa nini huwaheshimu wale wanaotenda ukweli, na mbona unawafuata mara moja wale wasiotenda ukweli punde kwa kuwaangalia tu? Je, hili ni tatizo la aina gani?

Sijali iwapo una ufahamu au la, sijali kwamba umelipa gharama kuu kiasi gani, sijali kuwa nguvu zako ni kuu kiasi gani na sijali ikiwa wewe ni nyoka mwovu wa ndani ama kiongozi anayepeperusha bendera. Ikiwa nguvu zako ni kuu basi ni kwa ajili tu ya usaidizi wa nguvu za Shetani; ikiwa hadhi yako iko juu, basi ni kwa sababu kuna wengi waliokuzunguka wasiotenda ukweli; ikiwa hujafukuzwa basi ni kwa kuwa sasa sio wakati wa kazi ya kufukuza, bali ni wakati wa kazi ya kuondoa. Hakuna haraka ya kukufukuza sasa. Ninasubiri tu siku ambayo Nitakuadhibu baada ya wewe kuondolewa. Yeyote asiyetenda ukweli ataondolewa!

Wale wanaomwamini Mungu kwa kweli ni wale walio tayari kuweka neno la Mungu kwenye matendo, na ni wale walio radhi kutenda ukweli. Wale wanaoweza kwa kweli kuwa shahidi kwa Mungu pia ni wale walio radhi kuweka neno Lake kwenye matendo, na ni wale ambao kwa kweli wanaweza kusimama upande wa ukweli. Wale wanaotumia hila na wale wanaotenda yasio haki wote ni watu wasiokuwa na ukweli na wote huleta aibu kwa Mungu. Wale walio kanisani wanaohusika na mabishano ni vibaraka wa Shetani, na ni mfano mwema wa Shetani. Mtu wa aina hii ni mwovu sana. Wale wasio na ufahamu na wasio na uwezo wa kusimama upande wa ukweli wanahifadhi nia mbovu na kufifisha ukweli. Watu hawa hata zaidi ni waakilishi kamili wa Shetani; wamepita hali ya ukombozi na ni wazi mno kuwa wao wote ni vitu vya kuondolewa. Wale wasiotenda ukweli hawapaswi kuruhusiwa kusalia katika familia ya Mungu, wala wale wanaobomoa kanisa kwa makusudi. Lakini sasa Sifanyi kazi ya kufukuza. Watafichuliwa tu na kuondolewa mwishoni. Hakuna kazi nyingine ya bure itakayofanywa kwa watu hawa; wale walio wa Shetani hawana uwezo wa kusimama upande wa ukweli, ilhali wale wanaotafuta ukweli wanaweza kusimama upande wa ukweli. Wale wasiotenda ukweli hawastahili kusikia njia ya kweli na hawastahili kuwa na ushuhuda kwa ukweli. Kimsingi ukweli si kwa ajili ya masikio yao lakini badala yake unazungumzwa kwa ajili ya masikio ya wale wanaoutenda. Kabla ya mwisho wa kila mtu kufichuliwa, wale wanaovuruga kanisa na kukatiza kazi kwanza wataachwa upande moja. Pindi kazi itakapokamilika, watu hawa watafunuliwa mmoja baada ya mwingine kabla ya kuondolewa. Wakati wa kutoa ukweli, Siwatilii maanani kwa sasa. Ukweli wote unapofichuliwa kwa mwanadamu watu hao wanapasa kuondolewa, kwa kuwa huo pia utakuwa wakati ambapo watu wataainishwa kulingana na aina yao. Kwa sababu ya werevu wao mdogo, wale wasio na ufahamu watakuja kuangamia mikononi mwa watu waovu na watapotoshwa na watu waovu na watashindwa kurudi. Watu hawa wanapasa kushughulikiwa kwa njia hii, kwa kuwa hawaupendi ukweli, kwa sababu hawana uwezo wa kusimama upande wa ukweli, kwa sababu wanawafuata watu waovu, wanawaunga mkono watu waovu, na kwa sababu wanashirikiana na watu waovu na kumuasi Mungu. Wanajua vema kuwa watu hao waovu wananururisha uovu lakini wanafanya mioyo yao kuwa migumu na kuwafuata, wakienda kinyume na ukweli. Je, watu hawa wasiotenda ukweli lakini wanaofanya mambo ya uharibifu na

ya chukizo wote si wanafanya maovu? Ingawa kuna wale miongoni mwao ambao wanajipa mtindo wenyewe kama “wafalme” na wale wanaofuata msururu nyuma yao, je, asili yao ya kuasi Mungu si ni sawa yote? Je, wanaweza kutoa sababu gani kuwa Mungu hawaokoi? Je, wanaweza kutoa sababu gani kuwa Mungu si mwenye haki? Je, si ni uovu wao wenyewe ambao umewaangamiza? Je, si ni uasi wao ambao utawavuta hadi jahanamu? Wale wanaotenda ukweli mwishowe wataokolewa na kufanywa wakamilifu kwa kupitia ukweli. Wale wasiotenda ukweli mwishowe watakaribisha maangamizi kwa kupitia ukweli. Hii ndio miisho inayowasubiri wale wanaotenda ukweli na wale wasioutenda. Ninawashauri wale ambao hawana mpango wa kutenda ukweli watoke kanisani haraka iwezekanavyo ili kuepuka kutenda dhambi nyingi zaidi. Wakati utakapofika, hata majuto yatakuwa yamechelewa, na hasa wale wanaofanya magenge na kufanya migawanyiko, na wale nyoka waovu wa ndani katika kanisa lazima watoke haraka sana. Watu hawa ambao ni wenye asili ya mbwa mwitu mwovu hawana uwezo wa mabadiliko, ni heri watoke kanisani kwa nafasi inayopatikana mwanzo, wasiweze kuyavuruga maisha mazuri ya ndugu tena, na hivyo kuepuka adhabu ya Mungu. Nyinyi ambao mlienda pamoja nao mtafanya vema kutumia nafasi hii kutafakari juu yenu wenyewe. Je, mtawafuata waovu nje ya kanisa, ama kusalia na kufuata kwa unyenyekevu? Lazima uzingatie jambo hili kwa makini. Ninawapa nafasi moja zaidi ya kuchagua. Ninalisubiri jibu lenu.

Unapaswa Kudumisha Ibada Yako kwa Mungu

Roho Mtakatifu Anafanya kazi vipi katika kanisa sasa? Je, una ufahamu wa hilo? Ni matatizo gani makubwa zaidi yanayowakumba ndugu na dada? Wamepungukiwa na nini zaidi? Kwa sasa, kuna watu ambao wako hasi katikati ya majaribio, na wengine wao hata wanalalamika, na wengine hawasongi mbele tena kwa sababu Mungu Hazungumzi tena. Watu hawajaingia njia sahihi ya imani katika Mungu. Hawawezi kuishi wakijitegemea, na hawezi kudumisha maisha yao ya kiroho. Kuna watu wengine ambao wanafuata, wanaofuatilia kwa nguvu, na wako tayari kutenda Mungu Akinena. Lakini Mungu Asiponena, hawasongi mbele tena. Watu bado hawajaelewa mapenzi ya Mungu katika mioyo yao na hawana mapenzi kwa Mungu moja kwa moja; kufuata kwao Mungu hapo awali ilikuwa kwa sababu walikuwa wamelazimishwa. Sasa kuna watu ambao wamechoka na kazi ya Mungu. Je, hawako hatarini? Watu wengi wako katika hali ya kuvumilia tu. Ingawa wanakula na kunywa maneno ya Mungu na kumuomba, yote ni kwa kusitasita. Hawana bidii waliyokuwa nayo mwanzoni, na watu wengi hawana shauku katika kazi ya Mungu ya uboreshaji na ukamilisho. Ni kana kwamba hawana bidii ya ndani kamwe, na wanalemewa na maasi hawahisi kuwa wana deni kwa Mungu, wala hawajuti wenyewe. Hawaufuatili ukweli ama kuondoka kanisani. Wanafuata tu raha za muda. Huyu ni aina ya mjinga mkuu wa kipumbavu! Wakati utakapofika, wote watatupwa nje, na hakuna mmoja atakayeokolewa! Je, unafikiri kuwa kama mtu ameokolewa mara moja

ataokolewa kila wakati? Hii ni kujaribu tu kuwapumbaza watu! Wale wote wasiofuata kuingia katika maisha wataadibiwa. Watu wengi hawana shauku hata kidogo ya kuingia katika maisha, katika maono, ama kuweka ukweli katika matendo. Hawafuati kuingia ndani, na kwa hakika hawafuati kuingia ndani zaidi. Je, hawajiangamizi wenyewe? Wakati huu, kuna sehemu ya watu ambao hali zao zinaendelea kuwa nzuri na nzuri zaidi. Roho Mtakatifu Anapofanya kazi zaidi, wanajiamini zaidi, na wanapozoea zaidi ndipo wanapohisi siri ya kushangaza ya kazi ya Mungu. Wanapoingia ndani zaidi, ndipo wanaelewa zaidi. Wanahisi kuwa upendo wa Mungu ni mkubwa sana, na wanahisi imara na kupata nuru ndani. Wana uelewa wa kazi ya Mungu. Hawa ni watu ambao Roho Mtakatifu Anafanya kazi ndani yao. Watu wengine wanasema, “Ingawa hakuna maneno mapya kutoka kwa Mungu, lazima bado niendeleo kuingia ndani katika ukweli, lazima niwe na bidii katika kila kitu katika mazoea yangu na kuingia katika ukweli wa maneno ya Mungu.” Mtu kama huyu ana kazi ya Roho Mtakatifu. Ingawa Mungu Haonyeshi uso Wake na Amejifichika kutoka kwa kila mtu, na Haneni neno lolote, na kuna nyakati ambazo watu wanapitia usafishaji wa ndani, ilhali Mungu hajawaacha watu Wake kabisa. Kama mtu hawezi kudumisha ukweli ambao anafaa kutekeleza, hatakuwa na kazi ya Roho Mtakatifu. Katika wakati wa usafishaji, wa Mungu kutojionyesha, kama hujiamini na unaogopa, usipo lenga kuwa na uzoefu wa maneno Yake, hii ni kutoroka kutoka kwa kazi ya Mungu. Baadaye, utatupwa nje. Wale ambao hawatafuti kuingia katika neno la Mungu hawana uwezo wa kusimama kama shahidi Wake. Watu ambao wanaweza kutoa ushahidi kwa Mungu na kuridhisha mapenzi Yake wote wanategemea kikamilifu bidii yao kufuatilia maneno ya Mungu. Kazi ambayo Mungu Anaitekeleza katika watu ni kimsingi kuwawezesha kuupata ukweli; Kukufanya wewe kufuatilia maisha ni kwa ajili ya kukukamilisha, na yote ni ya kukufanya ufae kutumika na Mungu. Yote unayofuata sasa ni kusikia siri, kusikiliza maneno ya Mungu, kulisha macho yako, kuona kitu kipya ama kuona ni mwenendo upi, na kuridhisha udadisi wako. Kama hii ndio nia ya moyo wako, hakuna vile utafikia mahitaji ya Mungu. Wale ambao hawafuati ukweli hawezi kufuata mpaka mwisho kabisa. Wakati huu, si kwamba Mungu hafanyi kitu—ni kwamba watu hawashirikiani, kwa sababu wamechoka na kazi Yake. Wanataka tu kusikia maneno ya baraka Yake, na hawataki kusikia maneno ya hukumu Yake na kuadibiwa. Sababu ya hii ni nini? Ni kwa sababu tamaa ya watu kupata baraka haijatimizwa, na wako hasi na wanyonge. Si kwamba Mungu kimakusudi hakubali watu kumfuata, na si kwamba anapeana mapigo kimakusudi kwa wanadamu. Watu wako hasi na wanyonge kwa sababu nia zao hazifai. Mungu ni Mungu Ambaye Anampa mwanadamu maisha, naye hawezi kumleta mwanadamu katika kifo. Uhasi wa watu, unyonge na kurudi nyuma yote yanasababishwa na wao wenyewe.

Kazi ya Mungu ya sasa inawaletea watu usafishaji kiasi, na wale tu ambao wanaweza kusimama imara katika usafishaji huu watapata kibali cha Mungu. Haijalishi ni jinsi gani

Anajificha, bila kuongea, ama kufanya kazi, bado unaweza kufuata kwa bidii. Hata kama Mungu Alisema angekukataa, bado ungemfuata Yeye. Hii ni kusimama kama shahidi kwa Mungu. Mungu Akijificha kutoka kwako nawe ukome kumfuata, hii ni kusimama shahidi kwa Mungu? Watu wasipoingia ndani kwa kweli, hawana kimo cha kweli, na wanapokabiliana na jaribio kubwa hasa, wanaanguka. Mungu haneni kwa sasa, ama kile Afanyacho hakilingani na dhana zako, kwa hivyo hauko sawa. Kama Mungu angekuwa sasa anatenda kulingana na dhana zako kwa sasa, kama Angekuwa anayakidhi matakwa yako na ukawa na uwezo wa kusimama na kufuatilia kwa nguvu, basi ni nini ambacho kweli ungekuwa unatumia kuendelea kuishi? Nasema kuwa kuna watu wengi ambao wanaishi wakitegemea kabisa udadisi wa binadamu. Hawana kabisa moyo wa kweli wa kufuata. Wale wote wasiofuata kuingia katika ukweli lakini wanategemea udadisi wao katika maisha ni watu wenye kustahili dharau walio hatarini! Kazi za Mungu tofauti yote ni ya kuwakamilisha wanadamu. Hata hivyo, watu daima ni wadadisi, wanapenda kuuliza kuhusu tetesi, wana wasiwasi kuhusu kinacho endelea nje ya nchi—ni nini kinaendelea Israeli, kama kuna mtetemeko wa ardhi Misri—kila wakati wanatafuta kitu mpya, kitu kisicho cha kawaida kuridhisha tamaa zao za kibinafsi. Hawafuati maisha, wala kufuata kukamilishwa. Wanatafuta tu siku ya Mungu kufika haraka ili ndoto yao nzuri ijulikane na tamaa zao badhirifu zitimie. Mtu kama huyo si wa kweli—ni mtu aliye na mtazamo usio sawa. Kuufuata ukweli ni msingi wa imani ya wanadamu katika Mungu. Watu wasipofuata kuingia katika maisha, wasipotafuta kumridhisha Mungu, basi watatiishwa chini ya adhabu. Wale watakoadhibiwa ni wale ambao hawajakuwa na kazi ya Roho Mtakatifu katika wakati wa kazi ya Mungu.

Watu wanafaa kushirikiana na Mungu vipi katika hatua hii ya kazi Yake? Mungu Anawajaribu watu kwa wakati huu. Haneni neno lolote; Anajificha na Hawasiliani na watu moja kwa moja. Kutoka nje, inaonekana kama Hafanyi kazi, lakini ukweli ni kwamba bado Anafanya kazi ndani ya mwanadamu. Yeyote anayefuatilia kuingia katika maisha ana maono kwa kufuata kwake maisha, na hana mashaka, hata kama haelewi kazi ya Mungu kikamilifu. Katikati ya majaribu, hata kama hajui ni nini Mungu Anataka kufanya na kazi gani Anataka kukamilisha, unafaa kujua kuwa nia za Mungu kwa wanadamu ni nzuri kila wakati. Ukimfuata na moyo wa kweli, Hatawahi kukuacha, na mwishowe kwa kweli Atakukamilisha, na kuwaleta watu katika mwisho unaofaa. Haijalishi ni vipi Mungu Anawajaribu watu kwa sasa, kuna siku moja ambayo Atawatolea watu matokeo yanayofaa na kuwapa adhabu inayofaa kulingana na kile ambacho wamefanya. Mungu Hatawaongoza watu hadi kituo fulani halafu Awatupe tu kando na kuwapuuza. Hii ni kwa sababu Yeye ni Mungu mwaminifu. Katika hatua hii, Roho Mtakatifu anafanya kazi ya usafishaji. Anamsafisha kila mmoja. Katika hatua za kazi zilizoundwa na majaribu ya kifo na majaribu ya kuadibu, usafishaji katika wakati huo ulikuwa usafishaji kupitia

maneno. Ili watu wapate uzoefu wa kazi ya Mungu, lazima kwanza waelewe kazi Yake ya sasa na kuelewa jinsi wanadamu wanafaa kushirikiana. Hili ni jambo ambalo kila mtu anafaa kuelewa. Haijalishi ni nini Mungu Anafanya, kama ni usafishaji ama kama Haneni, kila hatua ya kazi ya Mungu hailingani na dhana za wanadamu. Yote yanaenda mbali na kupenya katika dhana za watu. Hii ni kazi Yake. Lakini lazima uamini kwamba, kwa kuwa kazi ya Mungu imefika hatua fulani, Hatakubali wanadamu wote waangamie hata iweje. Anawapa ahadi na baraka kwa wanadamu, na wale wote wanaomfuata wataweza kupata baraka Yake, na wale wasiomfuata watatupwa nje na Mungu. Hii inategemea kufuata kwako. Haijalishi chochote, lazima uamini kuwa wakati kazi ya Mungu itakapomalizika, kila mtu atakuwa na mwisho unaofaa. Mungu Amewapa wanadamu matamanio mazuri, lakini wasipofuatilia, hawawezi kuyapata. Unafaa kuweza kuona hii sasa—Mungu kusafisha na kuwaadibu watu ni kazi Yake, lakini kwa watu, lazima wafuate badiliko katika tabia kila wakati. Katika mazoea yako ya kivitendo, lazima kwanza ujue jinsi ya kula na kunywa maneno ya Mungu; lazima upate kile unachofaa kuingia ndani na mapungufu yako ndani ya maneno Yake, utafute kuingia katika mazoea yako ya kivitendo, na uchukue sehemu ya kazi ya Mungu inayofaa kuwekwa katika matendo na ujaribu kuifanya. Kula na kunywa maneno ya Mungu ni kipengele kimoja, maisha ya kanisa lazima pia yadumishwe, lazima uwe na maisha ya kiroho ya kawaida, na uweze kumkabidhi Mungu hali zako zote za sasa. Haijalishi ni vipi kazi Yake inabadilika, maisha yako ya kiroho yanapaswa kubaki kawaida. Maisha ya kiroho yanaweza kudumisha kuingia ndani kwako kwa kawaida. Haijalishi kile ambacho Mungu Anafanya, unapaswa kuendeleza maisha yako ya kiroho bila kukatizwa na kutimiza wajibu wako. Hiki ndicho watu wanapaswa kufanya. Yote ni kazi ya Roho Mtakatifu, lakini huku kwa wale walio na hali ya kawaida huku ni kukamilishwa, kwa wale wasio na hali ya kawaida ni majaribu. Katika hatua ya sasa ya kazi ya Roho Mtakatifu ya kusafisha, watu wengine wanasema kuwa kazi ya Mungu ni kubwa sana na kwamba watu wanahitaji sana usafishaji, vinginevyo kimo chao kitakuwa ndogo sana na hawatakuwa na njia ya kufikia mapenzi ya Mungu. Hata hivyo, kwa wale walio na hali isiyo nzuri, inakuwa sababu ya kutomfuata Mungu, na sababu ya kutohudhuria mikusanyiko ama kula na kunywa neno la Mungu. Katika kazi ya Mungu, haijalishi ni nini Anafanya ama nini kinabadilika, kwa uchache sana watu lazima watu wadumishe hali ya chini zaidi ya maisha ya kawaida ya kiroho. Pengine umekuwa mwangalifu katika hatua hii ya sasa ya maisha yako ya kiroho, lakini bado hujapata mengi; hujavuna pakubwa. Katika hali za aina hizi lazima bado ufuate sheria; lazima ufuate sheria hizi ili usipate hasara katika maisha yako na ili uyakidhi mapenzi ya Mungu. Kama maisha yako ya kiroho si ya kawaida, huwezi kuelewa kazi ya sasa ya Mungu, badala yake kila wakati utahisi kwamba hayalingani kabisa na dhana zako mwenyewe, nawe una hiari ya kumfuata, lakini unakosa bidii ya ndani. Kwa hivyo haijalishi ni nini Mungu Anafanya sasa, lazima watu washirikiane. Watu wasiposhirikiana Roho Mtakatifu Hawezi kufanya kazi Yake,

na kama watu hawana moyo wa kushirikiana, basi si rahisi wao kupata kazi ya Roho Mtakatifu. Kama unataka kuwa na kazi ya Roho Mtakatifu ndani mwako, na kutaka kupata kibali cha Mungu, lazima udumishe moyo wako wa ibada asili mbele ya Mungu. Sasa, si lazima kwako kuwa na maelewano zaidi ya ndani, nadharia ya juu, ama vitu vingi—yote yanayohitajika ni kwamba ushikilie neno la Mungu juu ya msingi asili. Watu wasiposhirikiana na Mungu na wasipofuata kuingia zaidi, Mungu Atachukua kile walichokuwa nacho wakati mmoja. Ndani, watu wana tamaa kila wakati ya kilicho rahisi na afadhali wajifurahishe na kile ambacho kinapatikana. Wanataka kupata ahadi za Mungu bila kulipa gharama yoyote. Haya ni mawazo badhirifu ndani ya wanadamu. Kupata maisha yenyewe bila kulipa gharama—nini kimewahi kuwa rahisi? Mtu anapoamini katika Mungu na kutafuta kuingia katika maisha na kutafuta badiliko katika tabia yake, ni lazima aliye gharama na kufikia kiwango ambapo atamfuata Mungu daima bila kujali Anachofanya. Hiki ni kitu ambacho watu lazima wafanye. Hata kama unafuata haya yote kama sharti, ni lazima uyazingatie, na haijalishi majaribu yako ni makubwa kiasi gani, huwezi kuachilia uhusiano wako wa kufaa na Mungu. Unapaswa kuweza kuomba, udumishe maisha yako ya kanisa, na uishi na ndugu na dada. Mungu anapokujaribu, bado unapaswa kutafuta ukweli. Hiki ndicho kiwango cha chini cha maisha ya kiroho. Daima kuwa na moyo wa kutafuta na kujitahidi kushirikiana, kutumia nguvu zako zote—Je, hili linaweza kufanywa? Kwa msingi huu, utambuzi na kuingia katika uhalisi kitakuwa kitu ambacho unaweza kufanikisha. Ni rahisi kulikubali neno la Mungu wakati hali yako mwenyewe iko kawaida, na huhisi ugumu katika kuuweka ukweli katika matendo, na unahisi kuwa kazi ya Mungu ni kuu. Lakini kama hali yako ni duni, haijalishi kazi ya Mungu ni kuu vipi na haijalishi mtu anazungumza vizuri kivipi, hutasikiza chochote. Wakati hali ya mtu si ya kawaida, Mungu hawezi kufanya kazi ndani yao, na hawawezi kufanikisha mabadiliko katika tabia zao.

Kama watu hawana imani yoyote, sio rahisi kuendelea katika njia hii. Kila mtu sasa anaweza kuona kuwa kazi ya Mungu hailingani hata kidogo na fikira za watu. Mungu amefanya kazi nyingi sana na kuzungumza maneno mengi sana, ambayo hayalingani kabisa na dhana za binadamu. Hivyo, lazima watu wajiamini na wawe na utashi kuweza kusimama na kile wameshakiona na kile wamepata kutoka kwa uzoefu wao. Haijalishi ni nini Mungu Anafanya kwa watu, lazima washikilie kile walicho nacho, wawe waaminifu mbele za Mungu, na wasalie wenye kujitolea Kwake hadi mwisho. Huu ni wajibu wa wanadamu. Lazima watu watetee kile wanachopaswa kufanya. Imani katika Mungu inahitaji utiifu Kwake na uzoefu wa kazi Yake. Mungu Amefanya kazi nyingi sana—inaweza semekana kuwa kwa watu yote ni kukamilishwa, yote ni usafishaji, na hata zaidi, yote ni kuadibu. Hakujakuwa na hatua hata moja ya kazi ya Mungu ambayo imelingana na dhana za binadamu; kile watu wamefurahia ni maneno makali ya Mungu. Mungu Atakapokuja, watu wanapaswa kufurahia enzi Yake na hasira Yake, lakini

haijalishi maneno Yake yalivyo makali, Anakuja kuokoa na kukamilisha binadamu. Kama viumbe, watu wanapaswa watekeleze wajibu ambao wanafaa kufanya, na kusimama shahidi kwa Mungu katikati ya usafishaji. Katika kila jaribio wanapaswa washikilie ushahidi ambao wanapaswa washuhudie, na kushuhudia ushuhuda mkubwa kwa Mungu. Huyu ni mshindi. Haijalishi Mungu Anavyokuboresha, unabaki kuwa na imani kubwa na kutopoteza imani katika Mungu. Ufanye kile mwanadamu anafaa kufanya. Hiki ndicho Mungu Anahitaji kwa mwanadamu, na moyo wa binadamu unapaswa kuweza kurudi Kwake kikamilifu na kumwelekea katika kila wakati. Huyu ni mshindi. Wale wanaoitwa washindi na Mungu ni wale ambao bado wanaweza kusimama kama mashahidi, wakidumisha imani yao, na ibada yao kwa Mungu wanapokuwa chini ya ushawishi wa Shetani na kuzingirwa na Shetani, hiyo ni, wanapokuwa katika nguvu za giza. Kama bado unaweza kudumisha moyo wa utakaso na upendo wako wa kweli kwa Mungu kwa vyovyote vile, unasimama shahidi mbele ya Mungu, na hii ndio Mungu Anaita kuwa mshindi. Kama kufuata kwako ni bora kabisa Mungu Anapokubariki, lakini unarudi nyuma bila baraka Zake, si huu ni utakaso? Kwa sababu una uhakika kuwa njia hii ni ya kweli, lazima uifuata hadi mwisho; lazima udumishe ibada yako kwa Mungu. Kwa sababu umeona kuwa Mungu Mwenyewe amekuja duniani kukukamilisha, lazima umpe moyo wako Kwake kabisa. Haijalishi ni nini Anafanya, hata kama Anaamua tokeo lisilofaa kwako mwishowe, bado unaweza kumfuata. Hii ni kudumisha usafi wako mbele za Mungu. Kupeana mwili wa kiroho mtakatifu na bikira safi kwa Mungu inamaanisha kuweka moyo mwaminifu mbele za Mungu. Kwa wanadamu, uaminifu ni usafi, na kuweza kuwa mwaminifu kwa Mungu ni kudumisha usafi. Hii ndiyo unafaa kuweka katika matendo. Unapopaswa kuomba, omba; unapopaswa kukusanyika pamoja katika ushirika, fanya hivyo; unapopaswa kuimba nyimbo za kidini, imba nyimbo za kidini; na unapopaswa kuunyima mwili, unyime mwili. Unapotekeleza wajibu wako hulimalizi kwa kubahatisha; unapokumbana na majaribu unasimama imara. Hii ni ibada kwa Mungu. Usiposhikilia kile ambacho watu wanapaswa kufanya, basi kuteseka kwako na maazimio ya hapo awali yalikuwa ya bure.

Kwa kila hatua ya kazi ya Mungu, kunayo njia ambayo watu wanapaswa washirikiane. Mungu Anawasafisha watu ili wawe na imani katikati ya usafishaji. Mungu Anawakamilisha watu ili wawe na imani ya kukamilishwa na Mungu na wako tayari kuukubali usafishaji Wake na kushughulikiwa na kupogolewa na Mungu. Roho wa Mungu Anafanya kazi ndani ya watu ili kuwaletea nuru na mwangaza, na kuwafanya washirikiane Naye na kutenda. Mungu Haneni wakati wa usafishaji. Hatoi sauti Yake, lakini bado kuna kazi ambayo watu wanapaswa kuifanya. Unapaswa kushikilia kile ambacho unacho tayari, unapaswa bado kuwa na uwezo wa kumwomba Mungu, kuwa karibu na Mungu, na kusimama shahidi mbele ya Mungu; hivi utatimiza wajibu wako mwenyewe. Nyinyi wote mnapaswa muone kwa dhahiri kutoka kwa kazi

ya Mungu kuwa majaribu Yake ya imani ya watu na upendo inahitaji kuwa waombe zaidi kwa Mungu, na kwamba waonje maneno ya Mungu mbele Zake mara kwa mara. Mungu Akikupa nuru na kukufanya kuelewa mapenzi Yake lakini huyaweki katika matendo hata kidogo, hutapata chochote. Unapoyaweka maneno ya Mungu katika matendo, unapaswa bado kuwa na uwezo wa kumwomba, na unapoyaonja maneno Yake unapaswa utafute kila wakati mbele Zake na uwe umejaa imani Kwake bila kuvunjika moyo ama kuwa baridi. Wale wasioweka maneno ya Mungu katika matendo wamejawa na nguvu katika mikusanyiko, lakini wanaanguka katika giza wanaporudi nyumbani. Kuna wengine ambao hawataki hata kukusanyika pamoja. Kwa hivyo lazima uone kwa wazi ni wajibu gani ambao watu wanapaswa kutimiza. Unaweza kukosa kujua mapenzi ya Mungu ni nini hasa, lakini unaweza kutekeleza wajibu wako, unaweza kuomba inapopaswa, unaweza kuuweka ukweli katika matendo unapopaswa, na unaweza kufanya kile watu wanapaswa kufanya. Unaweza kushikilia maono yako asili. Hivi, utaweza kukubali zaidi hatua ya Mungu inayofuata. Ni shida ukikosa kutafuta wakati ambapo Mungu anafanya kazi katika njia iliyofichika. Anaponena na kuhubiri katika mabaraza, unasikiza kwa shauku, lakini Asiponena unakosa nguvu na kurudi nyuma. Mtu wa aina gani anafanya hivi? Huyu ni mtu ambaye tu anaenda na mkondo. Hana msimamo, hawana ushuhuda, na hawana maono! Watu wengi wako hivyo. Ukiendelea katika njia hiyo, siku moja utakapopitia jaribio kuu, utateremka katika adhabu. Kuwa na msimamo ni muhimu sana katika kukamilishwa kwa watu na Mungu. Kama huna shaka na hatua yoyote ya kazi ya Mungu, unatimiza wajibu ya mwanadamu, unashikilia kwa uaminifu kile Mungu Amekufanya ukiweke katika matendo, hiyo ni, unakumbuka mawaidha ya Mungu, na haijalishi Anachokifanya sasa husahau mawaidha Yake, huna shaka kuhusu kazi Yake, unadumisha msimamo wako, kushikilia ushahidi wako, na una ushindi katika kila hatua ya njia, mwishowe utakamilishwa kuwa mshindi na Mungu. Kama unaweza kusimama imara katika kila hatua ya majaribu ya Mungu, na bado unaweza kusimama imara hadi mwisho kabisa, wewe ni mshindi, na wewe ni mtu ambaye amekamilishwa na Mungu. Kama huwezi kusimama imara katika majaribu yako ya sasa, baadaye itakuwa hata vigumu zaidi. Ukipitia mateso kidogo yasiyo ya muhimu na usiufuate ukweli, hutapata chochote mwishowe. Utakuwa mkono mtupu. Kuna watu wengine ambao wanaacha kufuata wanapoona kuwa Mungu Haneni, na moyo wao unatawanyika. Je, si huyo ni mjinga? Watu wa aina hii hawana ukweli. Mungu Anenapo, wanakimbia huku na kule kila wakati, wakiwa na shughuli nyingi na kuwa na shauku kwa nje, lakini sasa Haneni, hawatafuti tena. Mtu kama huyu hana maisha ya usoni. Katika usafishaji, lazima uingie ndani kutoka kwa mtazamo halisi na usome masomo unayostahili kusoma; unapomwomba Mungu na kusoma neno Lake, unapaswa kulinganisha hali yako mwenyewe nayo, utambue pungufu zako, na ujue kuwa una somo mengi sana unayofaa kusoma. Unapotafuta kwa uaminifu katikati ya usafishaji, ndipo utakapojipata kuwa una pungufu. Unapokuwa unapitia usafishaji kunayo masuala mengi ambayo unapitia;

hautayaona kwa wazi, unalalamika, unatambulisha mwili wako wenyewe—ni kwa njia hii pekee ndiyo unaweza kugundua kwamba una tabia nyingi sana potovu ndani yako.

Watu wanakosa kwa tabia na wanaanguka mbali na kanuni za Mungu, baadaye wanaweza hata kuhitaji imani zaidi ili kutembea njia hii. Kazi ya Mungu katika siku za mwisho inahitaji imani kubwa—inahitaji imani kubwa zaidi hata kuliko ile ya Ayubu. Bila imani, watu hawataweza kuendelea kupata mazoea na hawataweza kukamilishwa na Mungu. Siku itakapokuja ambapo majaribu makuu yanakuja, watu wengine wataondoka kutoka kanisa hili, na wengine wataondoka kutoka kanisa lile. Kutakuwa na wengine ambao walikuwa wakifanya vizuri kiasi katika kufuata kwao katika siku za awali na haiko wazi mbona hawaamini tena. Vitu vingi vitafanyika na hutajua ni nini kinaendelea, na Mungu Hataonyesha dalili zozote ama ishara, ama kufanya chochote kisicho cha kawaida. Hii ni kuona kama unaweza kusimama imara—Mungu Anatumia ukweli kuwasafisha watu. Bado hujateseka sana. Hapo baadaye majaribu makuu yajapo, katika sehemu zingine kila mtu katika kanisa ataondoka, na wale umesikizana nao vizuri sana wataondoka na kuiacha imani yao. Utaweza kusimama imara wakati huo? Sasa, yale majaribu umepitia yamekuwa madogo, na pengine imekuwa vigumu kuyahimili. Hatua hii inajumuisha usafishaji na kukamilishwa kupitia neno pekee. Katika hatua inayofuata, ukweli utakuja juu yako kukusafisha, halafu utakuwa katikati ya hatari. Inapokuwa kubwa sana, Mungu Atakushauri uharakishe na uondoke, na watu wa kidini watajaribu kukushawishi ujunge. Hii ni ili kuona kama unaweza kuendelea katika njia hiyo. Haya yote ni majaribu. Majaribu ya sasa ni madogo, lakini siku itakuja ambapo kunao wazazi nyumbani ambao hawaamini tena na kunao watoto nyumbani ambao hawaamini tena. Je, utaweza kuendelea mbele? Unapoenda mbele zaidi, ndivyo majaribu yako yanakuwa mengi zaidi. Mtu Anatekeleza kazi Yake ya kuwasafisha watu kulingana na mahitaji yao na kimo chao. Katika hatua ya Mungu kuwakamilisha wanadamu, haiwezekani kuwa idadi ya watu itaendelea kukua—itapunguka tu. Ni kwa kupitia usafishaji huu tu ndipo watu wataweza kukamilishwa. Kushughulikiwa, kuadhibiwa, kujaribiwa, kuadibiwa, kulaaniwa—ndipo unaweza kustahimili haya yote? Unapoona kanisa lililo na hali nzuri hasa, ndugu na dada wote wanatafuta kwa nguvu kubwa, wewe mwenyewe unahisi umetiwa moyo. Siku ikija ambapo wote wameondoka, wengine wao hawaamini tena, wengine wameondoka kufanya biashara ama kuolewa, na wengine wamejiunga na dini, utaweza kusimama imara wakati huo? Je, utaweza kubaki bila mabadiliko ndani? Kukamilishwa kwa wanadamu kwa Mungu siyo jambo rahisi! Anatumia vitu vingi kuwasafisha watu. Watu wanaona haya kama mbinu, lakini kwa nia asili ya Mungu hizi sizo mbinu hata kidogo, ila ni ukweli. Mwishowe, Atakapokuwa Amewasafisha watu kufikia kiwango fulani na hawana malalamishi yoyote tena, hatua hii ya kazi Yake itakuwa imekamili. Kazi kuu ya Roho Mtakatifu ni kukukamilisha, na wakati ambapo Hafanyi kazi na Anajificha, hata zaidi ni kwa

sababu ya kukukamilisha, na hivi inaweza kuonekana hasa kama watu wana upendo kwa Mungu, na kama wana imani ya kweli Kwake. Mungu Anaponena wazi, hakuna haja ya wewe kutafuta; ni wakati tu ambapo Amejificha ndipo unahitaji kutafuta, unahitaji kuhisi njia yako hadi upite. Unapaswa kuweza kutimiza wajibu wa kiumbe aliyeumbwa, na haijalishi matokeo yako ya usoni na hatima yako inaweza kuwa ipi, unapaswa kuweza kufuatilia maarifa na upendo kwa Mungu katika miaka ambayo uko hai, na haijalishi jinsi Mungu anavyokutendea, unapaswa kuweza kuepuka kulalamika. Kuna sharti moja kwa kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya watu. Bora wana hamu na wanatafuta na hawasisiti ama kuwa na shaka kuhusu matendo ya Mungu, nao wanaweza kushikilia wajibu wao kila wakati, hivi tu ndivyo wanaweza kupata kazi ya Roho Mtakatifu. Katika kila hatua ya kazi ya Mungu, kinachohitajika kwa wanadamu ni imani kuu na kutafuta mbele za Mungu—kupitia tu kwa mazoea ndipo watu wataweza kugundua jinsi Mungu Anavyopendeka na jinsi Roho Mtakatifu Anavyofanya kazi ndani ya watu. Usipopata uzoefu, usipoihisi njia yako kupitia hayo, usipotafuta, hutapata chochote. Lazima uhisi njia yako kupitia mazoea yako, na kwa kupitia mazoea yako tu ndipo utaona matendo ya Mungu, na kugundua maajabu Yake na mambo Yake yasiyoeleweka.

Je, Wewe ni Mtu Ambaye Amepata Uzima?

Ni wakati tu ambapo umetupa tabia zako potovu na kutimiza kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida ndiyo utafanywa kuwa mkamilifu. Ingawa utakuwa huwezi kunena unabii, wala siri zozote, utakuwa unaishi kulingana na kufichua taswira ya mwanadamu. Mungu alimuumba mwanadamu, baada ya hapo mwanadamu akaharibiwa na Shetani, na uharibifu huu umewafanya watu wawe “maiti”—na hivyo, baada ya kuwa umebadilika, utakuwa tofauti na maiti hizi. Ni maneno ya Mungu ndiyo yanatoa uzima kwa roho za watu na kuwasababisha kuzaliwa upya, na roho za watu zinapozaliwa upya, watakuwa hai tena. Neno “wafu” linarejelea maiti ambazo hazina roho, kwa watu ambao roho zao zimekufa. Roho za watu zinapowekewa uhai, wanakuwa hai tena. Watakatifu waliozungumziwa awali huashiria watu ambao wamekuwa hai, wale ambao walikuwa chini ya ushawishi wa Shetani lakini wakamshinda Shetani. Wateule wa China wamestahimili ukatili na mateso na ulaghai wa joka kuu jekundu, ambalo limewaacha wakiwa wameharibika kiakili na kuwachwa wakiwa hawana hata ujasiri wa kuishi. Hivyo, kuamsha roho zao kunapaswa kuanza na hulka zao. Kidogo kidogo, katika hulka yao roho yao itaamshwa. Siku moja, watakapokuwa hai tena, hakutakuwa na vizuizi zaidi, na vyote vitasonga mbele bila tatizo. Kwa sasa, hii inabakia kuwa bado haijafanikiwa. Kuishi kwa kudhihirisha kwa watu wengi kunajumuisha mazingira ya kifo, wamezungukwa na hali ya kifo, na wamepungukiwa sana. Maneno ya baadhi ya watu yanabeba kifo, matendo yao yanabeba kifo, na takribani kila kitu wanachoishi kwa kudhihirisha ni kifo. Ikiwa leo, watu wanamshuhudia Mungu waziwazi, basi kazi hii itashindwa, maana bado hawajakuwa hai tena kikamilifu, na kuna wafu

wengi sana miongoni mwenu. Leo, baadhi ya watu wanauliza kwa nini Mungu haonyeshi ishara na maajabu ili kwamba aweze kusambaza kazi Yake miongoni mwa nchi za Wamataifa. Wafu hawawezi kuwa na ushuhuda wa Mungu; walio hai pekee ndio wanaweza, lakini watu wengi leo ni wafu, wengi wao wanaishi katika kifungo cha kifo, wanaishi chini ya ushawishi wa Shetani, na hawawezi kupata ushindi—na hivyo wanawezaje kuchukua ushuhuda wa Mungu? Wanawezaje kueneza kazi ya injili?

Wale wanaoishi chini ya ushawishi wa giza, ni wale ambao wanaishi katikati ya kifo, ni wale ambao wametawaliwa na Shetani. Bila kuokolewa na Mungu, na kuhukumiwa na kuadibiwa na Mungu, watu wanakuwa hawana uwezo kukwepa athari ya kifo, hawawezi kuwa hai. Wafu hawa hawawezi kuwa ushuhuda kwa Mungu, wala hawawezi kutumiwa na Mungu, wala kuingia katika ufalme. Mungu anataka ushuhuda wa walio hai, na sio wafu, na Anaomba kwamba walio hai, wala sio wafu, wamfanyie Yeye kazi. “Wafu” ni wale ambao wanampinga na kumwasi Mungu, ni wale ambao ni mbumbumbu katika roho na hawaelewi maneno ya Mungu, ni wale ambao hawawezi ukweli katika matendo na hawana utii hata kidogo kwa Mungu, na ni wale ambao wamemilikiwa na Shetani na kunyanyaswa na Shetani. Wafu wanajionyesha wenyewe kwa kuupinga ukweli, kwa kumwasi Mungu, na kwa kuwa duni, wa kudharaulika, kuwa waovu, katili, wadanganyifu, na kudhuru kwa siri. Ingawa watu wa namna hiyo wanakula na kunywa maneno ya Mungu, hawana uwezo wa kuishi kwa kudhihirisha maneno ya Mungu; wanaishi, lakini ni wafu wanaotembea, ni maiti zinazopumua. Wafu hawawezi kabisa kumridhisha Mungu, wala kumtii kikamilifu. Wanaweza tu kumdanganya, kusema maneno ya makufuru juu Yake, na kumsaliti, na yote wanayoyaishi kwa kudhihirisha hufichua asili ya Shetani. Ikiwa watu wanatamani kuwa viumbe hai, na kuwa na ushuhuda wa Mungu, na kuthibitishwa na Mungu, wanapaswa kukubali wokovu wa Mungu, wanapaswa kuwa watiifu katika hukumu na kuadibu Kwake, na wanapaswa kukubali kwa furaha kushughulikiwa na kupogolewa na Mungu. Ni hapo tu ndipo wataweza kuweka katika matendo ukweli wote unaohitajika na Mungu, na baada ya hapo ndipo wataweza kupata wokovu wa Mungu, na kuwa viumbe hai kabisa. Walio hai wanaokolewa na Mungu, wamehukumiwa na kuadibiwa na Mungu, wapo tayari kujitoa wenyewe na wana furaha kutoa maisha yao kwa Mungu, na wapo tayari kujitoa maisha yao yote kwa Mungu. Pale ambapo walio hai watachukua ushuhuda wa Mungu ndipo Shetani ataweza kuaibishwa, ni walio hai tu ndio wanaweza kueneza kazi ya injili ya Mungu, ni walio hai tu ndio wanaoupendeza moyo wa Mungu, ni walio hai tu ndio watu halisi. Mwanadamu wa asili aliyeumbwa na Mungu alikuwa hai, lakini kwa sababu ya uharibifu wa Shetani mwanadamu anaishi katikati ya kifo, na anaishi chini ya ushawishi wa Shetani, na hivyo watu hawa wamekuwa wafu ambao hawana roho, wamekuwa ni maadui ambao wanampinga Mungu, wamekuwa nyenzo ya Shetani, na wamekuwa mateka wa Shetani. Watu

wote walio hai ambao wameumbwa na Mungu wamekuwa wafu, na hivyo Mungu amepoteza ushuhuda wake, na Amempoteza mwanadamu, ambaye Alimuumba na ndiye kiumbe pekee aliye na pumzi Yake. Ikiwa Mungu ataamua kurejesha ushuhuda Wake, na kuwarejesha wale ambao waliumbwa kwa mkono wake lakini ambao wamechukuliwa mateka na Shetani, basi ni lazima awafufue ili waweze kuwa viumbe hai, na ni lazima awaongoe ili kwamba waweze kuishi katika nuru Yake. Wafu ni wale ambao hawana roho, wale ambao ni mbumbumbu kupita kiasi, na wale ambao wanampinga Mungu. Aidha, ni wale ambao hawamjui Mungu. Watu hawa hawana nia hata ndogo ya kumtii Mungu, kazi yao ni kumpinga na kuasi dhidi Yake, na hawana hata chembe ya utii. Walio hai ni wale ambao roho zao zimezaliwa upya, wale wanaojua kumtii Mungu, na ambao ni watii kwa Mungu. Wanao ukweli, na ushuhuda, na ni watu wa aina hii tu ndio wanaompendeza Mungu katika nyumba Yake. Mungu anawaokoa wale ambao wanaweza kuwa hai tena, ambao wanaweza kuuona wokovu wa Mungu, ambao wanaweza kuwa watii kwa Mungu, na wapo tayari kumtafuta Mungu. Anawaokoa wanaomwamini Mungu aliyepata mwili, na wanaamini katika kuonekana Kwake. Baadhi ya watu wanaweza kuwa hai tena, na baadhi hawawezi; inategemea na asili yao kama inaweza kuokolewa au la. Watu wengi wamesikia sana kuhusu maneno ya Mungu lakini bado hawaelewi mapenzi ya Mungu, wameyasikia maneno mengi sana ya Mungu lakini bado hawawezi kuyaweka katika vitendo, hawawezi kuishi kwa kudhihirisha ukweli wowote na pia kwa kukusudia kabisa wanaingilia kazi ya Mungu. Hawawezi kufanya kazi yoyote kwa ajili ya Mungu, hawawezi kujitolea chochote Kwake, na pia wanatumia kwa siri pesa za kanisa, na kula katika nyumba ya Mungu bure. Watu hawa ni wafu, na hawataokolewa. Mungu anawaokoa wale ambao wapo katika kazi Yake. Lakini kuna sehemu ya watu hao ambao hawawezi kupokea wokovu Wake; ni idadi ndogo tu ndiyo inaweza kupokea wokovu Wake. Hii ni kwa sababu watu wengi wamepotoshwa kwa kina sana na wakuwa wafu, na wamepita kiwango cha kuokolewa; wametumiwa vibaya kabisa na Shetani, na ni wenye hila sana katika asili yao. Watu hao wachache pia hawawezi kumtii Mungu kikamilifu. Hawakuwa wale ambao walikuwa waaminifu kabisa kwa Mungu tangu mwanzo, au wale ambao walikuwa na upendo wa hali ya juu kabisa kwa Mungu toka mwanzo; badala yake, wamekuwa watiifu kwa Mungu kwa sababu ya kazi Yake ya ushindi, wanamwona Mungu kwa sababu ya upendo wake mkuu, kuna mabadiliko katika tabia zao kwa sababu ya tabia ya Mungu ya haki, na wanamjua Mungu kwa sababu ya kazi Yake, ambayo ni halisi na ya kawaida. Bila kazi hii ya Mungu, haijalishi watu hawa ni wazuri kiasi gani bado wangebaki kuwa wa Shetani, bado wangukuwa ni wa kifo, bado wangukuwa wafu. Kwamba, leo, watu hawa wanaweza kupokea wokovu wa Mungu ni kwa sababu kabisa wanaweza kushirikiana na Mungu.

Kwa sababu ya utiifu wao kwa Mungu, walio hai wanaweza kuchukuliwa na Mungu na kuishi katika ahadi Zake, na kwa sababu ya upinzani wao kwa Mungu, wafu watachukiwa zaidi

na kukataliwa na Mungu na kuishi katikati ya adhabu na laana Zake. Hiyo ndiyo tabia ya haki ya Mungu, na haiwezi kubadilishwa na mwanadamu yeyote. Kwa sababu ya utafutaji wao wenyewe, watu wanapokea kibali cha Mungu na kuishi katika nuru; kwa sababu ya hila zao za kutisha, watu wanalaaniwa na Mungu, na kushuka chini katika adhabu; kwa sababu ya matendo yao maovu, watu wanaadhibiwa na Mungu; na kwa sababu ya kutamani kwao sana na utii wao, watu wanapokea baraka za Mungu. Mungu ni mwenye haki: Anawabariki walio hai, na kuwalaani wafu, ili kwamba siku zote wanakuwa katikati ya kifo, na kamwe hawataishi katika nuru ya Mungu. Mungu atawachukua walio hai kwenda katika ufalme Wake, Atawachukua walio hai kwenda katika baraka Zake milele. Wafu Atawaangusha katika kifo cha milele; wao ni wahusika wa uharibifu Wake, na siku zote watakuwa kwa Shetani. Mungu hamtendei mtu yeyote bila haki. Wale wote ambao kweli wanamtafuta Mungu hakika watabaki katika nyumba ya Mungu, na wale wote ambao hawamtii Mungu, na wale ambao hawana ulinganifu naye hakika wataishi katika adhabu Yake. Pengine huna uhakika kuhusu kazi ya Mungu katika mwili—lakini siku moja mwili wa Mungu hautapangilia hatima ya mwanadamu moja kwa moja; badala yake, Roho Wake, atapanga mwisho wa mwanadamu, na wakati huo watu watajua kwamba mwili wa Mungu na Roho Wake ni kitu kimoja, kwamba mwili Wake hauwezi kufanya kosa, na hata Roho Wake hawezi kabisa kufanya kosa. Na hatimaye, hakika atawachukua wale ambao watakuwa hai tena na kuwapeleka katika ufalme Wake, hakuna zaidi, wala pungufu, na wale wafu ambao hawakutoka wakiwa hai watatupwa katika shimo la Shetani.

Kuwa na Tabia Isiyobadilika Ni Kuwa katika Uadui na Mungu

Baada ya miaka elfu kadhaa ya upotovu, mwanadamu amekuwa asiyehisi na mpumbavu, pepo anayempinga Mungu, kwa kiasi kwamba uasi wa mwanadamu kwa Mungu umeandikwa katika vitabu vya historia, na hata mwanadamu mwenyewe hana uwezo wa kutoa ripoti kamili ya tabia zake za uasi wake—kwa kuwa mwanadamu amepotoshwa sana na Shetani, na amehadaiwa na Shetani kiasi kwamba hajui ni wapi pa kugeukia. Hata wa leo, mwanadamu bado anamsaliti Mungu: Wakati mwanadamu anamwona Mungu, anamsaliti, na wakati yeye hawezi kumwona Mungu, bado anamsaliti. Kuna hata wale ambao, baada ya kushuhudia laana ya Mungu na ghadhabu ya Mungu, bado wanamsaliti. Na hivyo Nasema kwamba hisia ya mwanadamu imepoteza kazi yake ya awali, na kwamba dhamiri ya mwanadamu, pia, imepoteza kazi yake ya awali. Mwanadamu Ninayemtazamia ni mnyama katika mavazi ya binadamu, yeye ni nyoka mwenye sumu, haijalishi jinsi anavyojaribu kuonekana mwenye kuhurumiwa machoni Pangu, Sitawahi kamwe kuwa na huruma kwake, kwa kuwa mwanadamu hana ufahamu wa kutofautisha kati ya nyeusi na nyeupe, tofauti kati ya ukweli na yasiyo ya kweli. Hisia ya mwanadamu ni usiohisi chochote, ilhali bado anataka apate baraka; ubinadamu wake si wa kuheshimika lakini bado anataka kumiliki ukuu wa mfalme. Ataweza kuwa mfalme wa nani, na hisia kama hiyo?

Jinsi gani yeye na ubinadamu kama huo ataweza kukaa kwenye kiti cha enzi? Mwanadamu kwa kweli hana aibu! Yeye ni mdhalili wa kujivuna tu! Kwa wale kati yenu mnaotaka kupokea baraka, Ninawashauri kwanza mtafute kioo na kuangalia picha zenu mbaya—je, una kile kinachohitajika kuwa mfalme? Je, una uso wa mwanadamu ambaye anaweza kupata baraka? Hakujawa mabadiliko hata madogo katika tabia yako na wewe hujaweka ukweli wowote katika vitendo, ilhali bado unatamani kuona siku ifuatayo ikiwa ya ajabu. Unajihadaa mwenyewe! Kwa sababu ya kuzaliwa katika nchi ya uchafu vile, mwanadamu ameangamizwa kabisa na jamii, amekuwa akishawishiwa na maadili ya kikabaila, na amefundisha katika “taasisi za elimu ya juu.” Fikra zilizo nyuma kimaendeleo, maadili potovu, mtazamo mbaya juu ya maisha, falsafa za kudharauliwa za kuishi, uwepo usio na thamani, na hali potovu za maisha na desturi—mambo yote haya yameuingilia moyo wa mwanadamu, na kudhoofisha na kushambuliwa dhamiri yake pakubwa. Matokeo yake, mwanadamu kamwe yuko mbali kutoka kwa Mungu, na kila mara anampinga. Tabia ya mwanadamu inakuwa matata zaidi kila siku, na hakuna hata mmoja ambaye kwa hiari yake atatoa chochote kwa ajili ya Mungu, hakuna hata mmoja ambaye kwa hiari atamtii Mungu, wala, zaidi ya hayo, mwanadamu mmoja ambaye kwa hiari yake atatafuta uso wa Mungu. Badala yake, chini ya umiliki wa shetani, mwanadamu hafanyi kitu ila kukimbiza anasa, kujitoa mwenyewe kwa upotovu wa mwili katika nchi ya matope. Hata wanaposikia ukweli, wale wanaoishi gizani hawafikiri kuuweka katika vitendo, na wala kuelekea kumtafuta Mungu hata kama wameuona mwonekano Wake. Jinsi gani wanadamu wapotovu kiasi hiki wawe na nafasi yoyote ya wokovu? Jinsi gani wanadamu waovu kiasi hiki kuishi katika mwanga?

Kubadilisha tabia ya mwanadamu huanza na maarifa ya kiini chake na kupitia mabadiliko katika mawazo yake, asili, na mtazamo wa akili—kwa njia ya mabadiliko ya msingi. Ni kwa njia hii tu ndio mabadiliko ya kweli yatapatikana katika tabia ya mwanadamu. Tabia ya upotovu ya mwanadamu inatokana na hali yake ya kupewa sumu na kukanyagwa na Shetani, kutokana na madhara mabaya sana ambayo Shetani ameweka katika mawazo yake, maadili, ufahamu, na hisia. Ni hasa kwa sababu mambo ya msingi ya mwanadamu yamepotoshwa na Shetani, na ni tofauti kabisa na jinsi Mungu aliwaumba kwa asili, kwamba mwanadamu humpinga Mungu na haelewi ukweli. Hivyo, mabadiliko katika tabia za mwanadamu lazima yaanze na mabadiliko katika mawazo yake, ufahamu na hisia ambayo yatabadilisha maarifa yake ya Mungu na maarifa yake ya ukweli. Wale waliozaliwa katika nchi potovu zaidi ndio wasiojua zaidi kumhusu kile Mungu Alichio, au kunamaanisha nini kumwamini Mungu. Jinsi watu walivyo wapotovu zaidi, ndivyo wanavyokosa kujua kuwepo kwa Mungu na ndivyo hisia zao na utambuzi huwa duni. Chanzo cha upinzani wa mwanadamu na uasi dhidi ya Mungu ni kupotoshwa kwake na Shetani. Kwa sababu amepotoshwa na Shetani, dhamiri ya mwanadamu imekuwa bila hisia, yeye ni

mwovu, mawazo yake yamepotoka, na ana mtazamo duni. Kabla ya kupotoshwa na Shetani, mwanadamu kawaida alimfuata Mungu na alitii maneno Yake baada ya kuyasikia. Alikuwa kawaida mwenye akili timamu na dhamiri, na wa ubinadamu wa kawaida. Baada ya kupotoshwa na Shetani, hali yake ya awali, dhamiri, na ubinadamu vilidhoofika sana na viliharibiwa na shetani. Hivyo, yeye amepoteza utii wake na upendo kwa Mungu. Akili ya mwanadamu imekuwa potovu, tabia yake imekuwa sawa na ile ya mnyama, na uasi wake kwa Mungu kabisa umekuwa wa mara kwa mara na wa kuhuzunisha zaidi. Hata hivyo mwanadamu bado hajui wala kutambua hili, na kwa upofu anapinga na kuasi. Ufunuo wa tabia ya mwanadamu ni udhihirisho wa hisia zake, utambuzi na dhamiri, na kwa sababu hisia yake na utambuzi si timamu, na dhamiri yake imezidi kuwa ndogo zaidi, hivyo tabia yake ni ya uasi dhidi ya Mungu. Kama hisia ya mwanadamu na utambuzi hauwezi kubadilika, basi mabadiliko katika tabia yake hayawezekani, sawa na kuwa baada ya moyo wa Mungu. Kama hisia ya mwanadamu sio timamu, basi hawezi kumhudumia Mungu na hafai kutumiwa na Mungu. “Hisia za Kawaida” inaashiria kutii na kuwa mwaminifu kwa Mungu, kuwa mwenye imani kamili kwa Mungu, na kwa kuwa na dhamiri kwa Mungu. Inamaanisha kuwa na moyo mmoja na akili kwa Mungu, na si kwa kumpinga Mungu kwa makusudi. Wale ambao ni wa akili potovu hawako hivi. Tangu mwanadamu aharibiwe na Shetani, ametunga dhana kuhusu Mungu, na yeye hajakuwa na uaminifu au kumtamani Mungu, pia hana dhamiri kwa Mungu. Mwanadamu kwa makusudi anapinga na huweka hukumu juu ya Mungu, na, zaidi ya hapo, anatupa shutuma Kwake nyuma Yake. Mwanadamu anajua vizuri kuwa Yeye ni Mungu, lakini bado humhukumu nyuma ya mgongo wake, hana nia ya kumtii, na hufanya madai ya kipofu na maombi kwa Mungu. Watu wa aina hii—watu walio na akili potovu—hawana uwezo wa kujua tabia zao za kudharauliwa au ya kujuta uasi wao. Kama watu wana uwezo wa kujijua wenyewe, basi wao wamerudisha kiasi kidogo cha akili zao; Zaidi ya vile watu wanavyomuasi Mungu lakini hawajui wenyewe, ndivyo walivyo zaidi wenye akili isiyo timamu.

Chanzo cha ufunuo wa upotovu wa tabia ya mwanadamu ni dhamiri yake iliyofifia, asili yake mbovu na akili yake isiyo timamu; kama dhamiri ya mwanadamu na hisia vinaweza kurudi kawaida, basi atafaa kwa matumizi mbele ya Mungu. Ni kwa sababu tu kuwa dhamiri ya mwanadamu daima imekuwa isiyosikia, akili ya mwanadamu haijawahi kuwa timamu, na inazidi kuwa hafifu ndio mwanadamu amezidisha uasi wake kwa Mungu, hata akampiga Yesu misumari juu ya msalaba na kumkataa Mungu mwenye mwili wa siku za mwisho kuingia katika nyumba yake, na analaani mwili wa Mungu, na anaona mwili wa Mungu kuwa wa hali ya chini. Kama mwanadamu angekuwa na ubinadamu kidogo, hangekuwa mkatili kiasi hicho katika utendeaji wake wa mwili wa Mungu mwenye mwili; kama angekuwa na akili hata kidogo tu, hangekuwa hivyo katika utendeaji wake wa mwili wa Mungu mwenye mwili; kama angekuwa na dhamiri

hata kidogo, hangekuwa mwenye “shukrani” kwa Mungu mwenye mwili kwa njia hii. Mwanadamu anaishi katika enzi ya Mungu kuwa katika mwili, lakini yeye hawezi kumshukuru Mungu kwa kumpatia nafasi nzuri kiasi hicho, na badala yake analaani kuja kwa Mungu, au kupuuza kabisa ukweli wa Mungu aliyepata mwili, na inaonekana anapinga hali hii na anachoshwa nayo. Haijalishi jinsi mwanadamu anachukua kuja kwa Mungu, Mungu, kwa ufupi, daima ameendeleza kazi yake kwa uvumilivu—hata kama mwanadamu hajawahi kumkaribisha, na bila kujua yeye hufanya maombi kwa Mungu. Tabia ya mwanadamu imekuwa mbaya zaidi, akili yake imekuwa hafifu zaidi, na dhamiri yake imekanyagwa kabisa na yule muovu na kwa muda mrefu imekoma kuwa dhamiri ya awali ya mwanadamu. Mwanadamu hajakosa tu shukrani kwa Mungu mwenye mwili kwa kukabidhi maisha na neema nyingi juu ya wanadamu, bali pia anachukia Mungu kwa kumpatia ukweli; ni kwa sababu mwanadamu hana haja ya kujua ukweli hata kidogo ndio maana anamchukia Mungu. Haitoshi kwamba mwanadamu hawezi kuutoa uhai wake kwa ajili ya Mungu mwenye mwili tu, lakini pia anajaribu kutoa neema kutoka kwa Mungu, na anafanya madai kwa Mungu yaliyo mara kadhaa kubwa kuliko kile mwanadamu ametoa kwa Mungu. Watu wa dhamiri na hisia kama hizo hufikiria kwamba hili si jambo kubwa, na bado wanaamini kuwa wao wamefanya mengi sana kwa ajili ya Mungu, na kwamba Mungu amewapa kidogo sana. Kuna watu ambao wamenipa bakuli la maji na kisha kunyosha mikono yao na kudai kwamba nilipie bakuli mbili za maziwa, au kunipa chumba kwa usiku mmoja lakini walijaribu kunilipisha mara nyingi zaidi katika ada ya makazi. Ukiwa na ubinadamu kama huo, na dhamiri ya aina hii, ni jinsi gani bado mnatarajia kupata uzima? Nyinyi ni fukara wa kudharauliwa mlioje! Ni kwa sababu ya ubinadamu huu na dhamiri ya mwanadamu ndio maana Mungu mwenye mwili anatembea katika ardhi yote, asipate mahali pa makazi. Wale ambao kwa kweli wanayo dhamiri na ubinadamu wanapaswa kumuabudu na kwa moyo wote kumhudumia Mungu mwenye mwili si kwa sababu ya kiasi cha kazi aliyofanya, lakini hata kama Yeye hangefanya kazi yoyote kamwe. Hili ndilo linafaa kufanywa na wale walio na akili timamu, na ndio wajibu wa mwanadamu. Watu wengi hata huzungumza juu ya masharti katika huduma yao kwa Mungu: Hawajali kama yeye ni Mungu au mwanadamu, na wao huzungumza juu ya masharti yao tu, na kutafuta kuridhisha tamaa zao wenyewe tu. Mnaponipikia, mnadai malipo ya huduma, wakati mnakimbia kwa ajili Yangu, mnadai pesa za mkimbiaji, mkinifanyia kazi mnadai ada ya kazi, mkifua nguo Zangu, mnadai ada ya kufua, wakati mnatoa kwa ajili ya kanisa mnadai malipo ya kurudisha nguvu, mkizungumza, mnadai malipo ya msemaji, mkipeana vitabu mnadai ada ya usambazaji, na wakati mnaandika mnadai malipo ya kuandika. Wale Nimehusiana nao hata hudai malipo kutoka Kwangu, na wale waliotumwa nyumbani hudai fidia kwa uharibifu wa majina yao; wale ambao hawajaoa au kuolewa hudai mahari, au fidia kwa ujana wao waliopoteza, wale wanaochinja kuku wanadai ada ya uchinjaji, wale wanaokaanga chakula wanadai ada ya kukaanga, na wale ambao hupika supu wanadai malipo pia.... Huu ndio

ubinadamu wenu mkuu na wenye majivuno, na haya ndiyo matendo yanayoamrisha na dhamiri yenu yenye joto. Hisia zenu ziko wapi? Ubinadamu wenu uko wapi? Wacha Niwaambie! Mkiendelea hivi Nitakoma kufanya kazi miongoni mwenu. Sitafanya kazi miongoni mwa wanyama waliovalia mavazi ya binadamu, Sitateseka hivyo kwa ajili ya kundi la watu ambao nyuso zao nzuri zimeficha nyoyo za uhasama, Sitavumilia kwa ajili ya kundi la wanyama ambao hawana uwezekano hata kidogo wa kuokolewa. Siku Nitakayowapa mgongo ndiyo siku mtakayokufa, ndiyo siku ambayo giza litakuja juu yenu, na ni siku mtakayoachwa na mwanga. Hebu Niwaambie! Sitakuwa mwema kamwe kwa kundi kama lenu, kundi ambalo liko chini ya hata wanyama! Kuna mipaka katika maneno na matendo Yangu, na vile ubinadamu wenu na dhamiri zilivyo, Sitafanya kazi zaidi, kwani mmekosa dhamiri, umenisababishia maumivu mengi sana, na tabia yenu ya kudharauliwa inanichukiza Mimi sana. Watu wanaokosa utu na dhamira kamwe hawatakuwa na nafasi ya wokovu; Mimi kamwe Sitawaokoa watu kama hao wasio na utu wala shukurani. Siku Yangu itakapofika, Nitanyesha mvua ya moto Wangu mkali milele juu ya wana waasi walioiamsha hasira na ghadhabu yangu kali hapo awali, Nitalazimisha adhabu yangu milele juu ya wanyama wale ambao wakati mmoja waliupa lugha chafu Kwangu na wakaniacha, Nitawachoma wakati wote kwa moto wa hasira Yangu wana wa uasi waliokula na kuishi pamoja Nami lakini hawakuniamini, na wakanitukana na kunisaliti. Nitawatia wote walionikasirisha kwa adhabu Yangu, Nitanyesha ghadhabu Yangu kwa ukamilifu juu ya wanyama hao waliotamani wakati mmoja kusimama kando Yangu kama visawe Vyangu ilhali hawakuniabudu wala kunitii, fimbo Ninayotumia kumgonga mwanadamu itaanguka juu ya wanyama hao waliofurahia utunzaji Wangu na siri Nilizonena, na waliojaribu kuchukua starehe ya mali ya dunia kutoka Kwangu. Sitamsamehe mtu yeyote anayejaribu kuchukua nafasi Yangu; Sitamsamehe yeyote anayejaribu kupokonya chakula na nguo kutoka Kwangu. Kwa sasa, mnabaki huru kutokana na madhara na kuendelea kujiharibia kwa kuzidi katika mahitaji mnayotaka kutoka Kwangu. Siku ya ghadhabu inapofika hamtafanya madai yoyote zaidi Kwangu; wakati huo, Nitawaruhusu “kujifurahia” hadi mtakaporidhika, Nitalazimisha nyuso zenu kuingia mchangani, na kamwe hamtaweza kuinuka tena! Wakati mmoja au mwingine, Ninaenda “kulipiza” madeni hayo kwenu na Natumaini mnasubiri kwa uvumilivu kuwasili kwa siku hii.

Kama viumbe hawa wa kudharauliwa wanaweza kweli kuweka kando tamaa zao kuu na kurudi kwa Mungu, basi wao bado wana nafasi ya wokovu; kama mwanadamu ana moyo ambao kwa kweli unamtamani Mungu, basi yeye hataachwa na Mungu. Mwanadamu anashindwa kumpata Mungu sio kwa sababu Mungu ana hisia, au kwa sababu Mungu hataki kupatikana na mwanadamu, bali ni kwa sababu mwanadamu hataki kumpata Mungu, na kwa sababu mwanadamu hana haraka kumtafuta Mungu. Jinsi gani mmoja wa wale ambao kweli

wanamtafuta Mungu alaaniwe na Mungu? Ni jinsi gani mwenye akili timamu na dhamiri nzuri anaweza laaniwa na Mungu? Ni vipi yule anayemwabudu kwa kweli na kumhudumia Mungu ataangamizwa na moto wa ghadhabu yake? Ni jinsi gani mwanadamu aliye na furaha ya kumtii Mungu kutupwa nje ya nyumba ya Mungu kwa mateke? Jinsi gani mwanadamu ambaye hawezi kumpenda Mungu vya kutosha aishi katika adhabu ya Mungu? Jinsi gani mwanadamu ambaye ana furaha ya kuacha kila kitu kwa ajili ya Mungu kuachwa bila chochote? Mwanadamu hana nia ya kumfuata Mungu, hana nia ya kutumia mali yake kwa Mungu, hana nia ya kutoa juhudi za milele kwa Mungu, na badala yake anasema kwamba Mungu amepita kiasi, kwamba mengi kuhusu Mungu yanakinzana na dhana za mwanadamu. Na ubinadamu kama huu, hata kama mngekuwa wakarimu katika juhudi zenu bado hamngeweza kupata kibali cha Mungu, bila kutaja kuwa hamumtafuti Mungu. Je, hamjui kwamba ninyi ni bidhaa mbovu za binadamu? Je, hamjui kwamba hakuna ubinadamu ulio mnyenyekevu zaidi kuliko wenu? Je, hamjui “cheo” chenu ni kipi? Wale ambao kweli wanampenda Mungu wanawaita baba wa mbweha, mama wa mbweha, mwanambweha, na mjukuu wa mbweha; nyinyi ni vizazi vya mbweha, watu wa mbweha, na mnapaswa kujua utambulisho wenu na kamwe msiwahi kuusahau. Msidhani kwamba nyinyi ni kiumbe mkubwa zaidi: Nyinyi ni kundi mojawapo la wasio-wanadamu wabaya zaidi miongoni mwa wanadamu. Je, hamjui lolote kuhusu haya? Je, mnajua ni kiasi gani cha hatari Nimechukua kwa kufanya kazi miongoni mwenu? Kama akili yenu haiwezi kurudi kawaida, na dhamiri yenu haiwezi kufanya kazi kwa kawaida, basi kamwe hamtawahi kuwa huru kutokana na jina “mbwa mwitu”, kamwe hamtatoroka siku ya laana, kamwe hamtatoroka siku ya adhabu yenu. Mlizaliwa mkiwa duni, kitu kisicho na thamani yoyote. Kwa hivyo nyinyi ni kundi la mbwa mwitu wenye njaa, rundo la uchafu na takataka, na, tofauti na nyinyi, Mimi Sifanyi kazi kwenu ili nipate chochote, lakini kwa sababu ya haja ya kazi. Mkiendelea kuwa waasi kwa njia hii, basi Nitakomesha kazi Yangu, na kamwe sitafanya kazi kwenu tena; badala yake, Nitahamisha Kazi yangu kwa kundi lingine linalonipendeza, na kwa njia hii kuondoka kwenu milele, kwa sababu Mimi sina nia ya kuwaangalia walio katika uadui na Mimi. Hivyo basi, je, mnataka kulingana na Mimi, au katika uadui dhidi Yangu?

Watu Wote Wasiomjua Mungu Ni Watu Wanaompinga Mungu

Kufahamu madhumuni ya kazi ya Mungu, athari inayotimizwa kwa mwanadamu, na mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu, hiki ndicho kitu ambacho kila mwanadamu anayemfuata Mungu anapaswa kutimiza. Sasa wanachokosa watu wote ni ufahamu wa kazi ya Mungu. Mwanadamu haelewi wala kufahamu kabisa maana ya vitendo vya Mungu ndani ya mwanadamu, kazi yote ya Mungu, na mapenzi ya Mungu tangu kuumbwa kwa dunia. Huu upungufu hauonekani tu katika ulimwengu mzima wa kidini, lakini zaidi ya hayo kwa waumini wote wa Mungu. Siku itakapofika utakapomtazama Mungu kwa kweli na kutambua hekima ya

Mungu; utakapotazama matendo yote ya Mungu na kutambua kile Mungu Alichona kile Alichona nacho; utakapotazama wingi Wake, hekima, ajabu Yake, na kazi Yake yote kwa mwanadamu, basi hapo ndipo utakuwa umefikia imani ya mafanikio kwa Mungu. Mungu anaposemekana kuwa Anayejumuisha yote na mwenye wingi, ni nini kinachomaanishwa na kujumuisha yote? Na nini kinachomaanishwa na utele? Iwapo huelewi haya, basi huwezi kuchukuliwa kuwa muumini wa Mungu. Mbona Nasema wale walio katika dunia ya kidini hawaamini katika Mungu na ni waovu, walio sawa na ibilisi? Ninaposema ni watenda maovu, ni kwa sababu hawaelewi matakwa ya Mungu, wala kuona hekima Yake. Hakuna wakati wowote ambao Mungu anadhihirisha kazi Yake kwao; ni vipofu, wasioona matendo ya Mungu. Wao ndio walioachwa na Mungu na hawamiliki kabisa utunzaji na ulinzi wa Mungu, sembuse kazi ya Roho Mtakatifu. Wale wasio na kazi ya Mungu ni watenda maovu na humpinga Mungu. Wale Ninaosema wanampinga Mungu ni wale wasiomjua Mungu, wale wanaokiri Mungu na maneno matupu ilhali hawamjui, wale wanaomfuata Mungu lakini hawamtii, na wale wanaofurahia neema ya Mungu lakini hawawezi kumshuhudia. Bila ufahamu wa madhumuni ya kazi ya Mungu na kazi ya Mungu kwa mwanadamu, mwanadamu hawezi kuwa katika ulinganifu na moyo wa Mungu, na hawezi kumshuhudia Mungu. Sababu kwamba mwanadamu humpinga Mungu inatoka, kwa upande mmoja, katika tabia potovu ya mwanadamu, na kwa upande mwingine, kutokana na kutomfahamu Mungu na kutoelewa kanuni za kazi ya Mungu na mapenzi Yake kwa mwanadamu. Vipengele hivi viwili vinaunganishwa katika historia ya upinzani wa mwanadamu kwa Mungu. Wanafunzi katika imani wanampinga Mungu kwa sababu upinzani kama huu uko ndani ya asili yao, ilhali upinzani dhidi ya Mungu wa wale walio na miaka mingi katika imani unatokana na kutomfahamu Mungu, kuongeza kwa tabia yao potovu. Kwa muda kabla ya Mungu kuwa mwili, kipimo cha kama mwanadamu alimpinga Mungu kilikuwa iwapo alishika amri zilizotolewa na Mungu mbinguni. Kwa mfano, katika Enzi ya Sheria, wowote ambao hawakushika sheria za Yehova walikuwa ndio wale waliompinga Mungu; wowote walioiba sadaka ya Yehova, na wowote waliosimama dhidi ya wale waliofadhiliwa na Yehova walikuwa wale waliompinga Mungu na wale ambao wangepigwa mawe hadi kufa; wowote ambao hawakuwaheshimu mama na baba zao, na wowote waliompiga ama kumlaani mwingine ni wale ambao hawakufuata sheria. Na wote ambao hawakufuata sheria za Yehova walikuwa wale waliosimama dhidi Yake. Hii haikuwa hivyo tena katika Enzi ya Neema, wakati wale waliosimama dhidi ya Yesu walikuwa wale waliosimama dhidi ya Mungu, na wowote ambao hawakutii maneno yaliyotamkwa na Yesu ni wale waliosimama dhidi ya Mungu. Katika enzi hii, makusudio ya upinzani kwa Mungu yalifafanuliwa zaidi na kuwa halisi. Kwa wakati ambao Mungu bado hakuwa amegeuka mwili, kipimo cha iwapo mwanadamu alimpinga Mungu kilitegemea iwapo mwanadamu alimwabudu na kumheshimu Mungu aliye mbinguni asiyeonekana. Ufafanuzi wa upinzani kwa Mungu wakati huo haukuwa halisi, kwani

mwanadamu wakati huo hangemwona Mungu wala kujua mfano wa Mungu ama jinsi Alivyofanya kazi na kuongea. Mwanadamu hakuwa na dhana za Mungu na alimwamini Mungu kwa njia isiyo dhahiri, kwani Hakuwa amejitokeza kwa mwanadamu. Kwa hivyo, vile mwanadamu alivyomwamini Mungu katika mawazo yake, Mungu hakumlaumu mwanadamu ama kuulizia mengi kutoka kwa mwanadamu, kwani mwanadamu hangemwona Mungu hata kidogo. Mungu anapopata mwili na kuja kufanya kazi miongoni mwa wanadamu, wote wanamtazama Mungu na kusikia maneno Yake, na wote wanaona vitendo ambavyo Mungu anafanya kutoka ndani ya mwili Wake wa nyama. Katika wakati huo, fikira zote za mwanadamu zinakuwa povu tu. Kwa wale wanaomwona Mungu anayejitokeza katika mwili, wote walio na utiifu ndani ya mioyo yao hawalaaniwi, ilhali wanaosimama dhidi Yake kimakusudi watachukuliwa kuwa wapinzani wa Mungu. Wanadamu kama hao ni maadui wa Kristo na ni maadui wanaosimama dhidi ya Mungu kimakusudi. Wale walio na dhana kumhusu Mungu lakini bado wanatii kwa furaha hawatalaaniwa. Mungu anamlaani mwanadamu kulingana na nia yake na vitendo vyake, kamwe sio kwa mawazo na fikira zake. Iwapo mwanadamu angelaaniwa kwa misingi hiyo, basi hakuna mmoja ambaye angeweza kutoroka kutoka katika mikono ya Mungu ya ghadhabu. Wale wanaosimama makusudi dhidi ya Mungu mwenye mwili wataadhibiwa kwa sababu ya kutotii kwao. Upinzani wao wa makusudi unatokana na dhana zao kumhusu, ambao unasababisha usumbufu wao kwa kazi ya Mungu. Wanadamu kama hao wanapinga na kuiharibu kazi ya Mungu wakijua. Hawana tu dhana za Mungu, lakini wanafanya kile kinachosumbua kazi Yake, na ni kwa sababu hii ndiyo wanadamu kama hao watahukumiwa. Wale wasioshiriki katika usumbufu wa kazi ya Mungu kimakusudi huwatahukumiwa kama wenye dhambi, kwani wanaweza kutii kwa bila kulazimishwa na kutosababisha vurugu na usumbufu. Wanadamu kama hao hawatahukumiwa. Hata hivyo, wakati wanadamu wamepata uzoefu wa miaka mingi ya kazi ya Mungu, kama bado wanaficha dhana zao za Mungu na kubaki wasioweza kujua kazi ya Mungu mwenye mwili, na licha ya miaka mingi ya uzoefu, wanaendelea kushikilia dhana nyingi za Mungu na bado hawawezi kuja kumjua Mungu, basi hata kama hawasababishi shida yoyote kukiwa na dhana nyingi za Mungu ndani ya mioyo yao, na hata kama dhana kama hizi hazionekani, wanadamu kama hao hawana huduma yoyote kwa kazi ya Mungu. Hawawezi kuhubiri injili wala kumshuhudia Mungu; wanadamu kama hao hawana manufaa na ni wapumbavu. Kwa sababu hawamjui Mungu na hawawezi kuondoa dhana zao za Mungu, wamelaaniwa. Inaweza kusemwa hivi: Si jambo geni kwa wanafunzi wa kidini kuwa na dhana za Mungu ama kutojua chochote kumhusu, lakini sio kawaida kwa wale walioamini kwa miaka mingi na kuwa na uzoefu mwingi wa kazi Yake kushikilia dhana kama hizi, na hata zaidi kwa wanadamu kama hao kutokuwa na ufahamu wa Mungu. Ni kwa sababu ya hali kama hii isiyo ya kawaida ndio wanadamu kama hao wanalaaniwa. Wanadamu wasio wa kawaida kama hao hawana manufaa; ni wale wanaompinga Mungu zaidi na waliofurahia neema ya Mungu bure.

Wanadamu wote kama hao wataondolewa mwishoni!

Wowote wasioelewa madhumuni ya kazi ya Mungu ni wale wanaompinga Mungu, na hata zaidi ya hayo ni wale waliofahamu madhumuni ya kazi ya Mungu lakini bado hawatafuti kumridhisha Mungu. Wale wanaosoma Biblia katika makanisa makubwa hukariri Biblia kila siku, lakini hakuna yeyote anayeelewa madhumuni ya kazi ya Mungu. Hakuna hata mmoja anayeweza kumwelewa Mungu; juu ya hayo, hakuna yeyote anayekubaliana na moyo wa Mungu. Wote hawana thamani, wanadamu waovu, kila mmoja akisimama juu kufundisha kuhusu Mungu. Ingawa wanalionyesha hadharani jina la Mungu, wanampinga kwa hiari. Ingawa wanajiita waumini wa Mungu, wao ni wale wanaokula mwili na kunywa damu ya mwanadamu. Wanadamu wote kama hao ni mashetani wanaoteketeza nafsi ya mwanadamu, pepo wakuu wanaowasumbua kimakusudi wanaojaribu kutembea katika njia iliyo sawa, na vizuizi vinavyozuia njia ya wanaomtafuta Mungu. Inagawa wao ni wenye “mwili imara,” wafuasi wao watajuaje kwamba wao ni wapinga Kristo wanaomwongoza mwanadamu katika upinzani kwa Mungu? Watajuaje kwamba hao ni mashetani hai wanaotafuta hasa nafsi za kuteketeza? Wale wanaojiheshimu mbele ya Mungu ni wanadamu wa chini kabisa, ilhali wanaojinyenyekeza ndio wa heshima zaidi. Na wale wanaojifikiria kujua kazi ya Mungu na kutangaza neno la Mungu kwa wengine kwa kishindo na tarumbeta nyingi wakati macho yao yako Kwake—hawa ndio wajinga zaidi kati ya wanadamu. Wanadamu kama hao ni wale wasio na ushahidi wa Mungu, na wale walio na kiburi na majivuno. Wale wanaoamini kwamba wana ufahamu mdogo wa Mungu licha ya uzoefu wao halisi na ufahamu wa vitendo ni wale Anaowapenda zaidi. Ni wanadamu kama hawa ndio walio na ushahidi wa kweli na wanaweza kweli kukamilishwa na Mungu. Wale wasioelewa mapenzi ya Mungu ni wapinzani wa Mungu; wale wanaoelewa mapenzi ya Mungu lakini bado hawauweki ukweli katika vitendo ni wapinzani wa Mungu; wale wanaokula na kunywa maneno ya Mungu lakini bado wanaenda dhidi ya kiini cha maneno ya Mungu ni wapinzani wa Mungu; wale walio na dhana za Mungu mwenye mwili na wanaasi makusudi ni wapinzani wa Mungu; wale wanaomhukumu Mungu ni wapinzani wa Mungu; na yeyote asiyeweza kumjua Mungu na kumshuhudia ni mpinzani wa Mungu. Kwa hivyo sikiliza ushawishi Wangu: Kama kweli una imani ya kutembea njia hii, basi zidi kuifuata. Iwapo huwezi kuepuka upinzani kwa Mungu, basi ni bora kwenda zako kabla hujachelewa. Vinginevyo, inaashiria mabaya badala ya mazuri, kwani asili yenu ni potovu sana. Huna uaminifu ama utii hata kidogo, ama moyo ulio na kiu ya haki na ukweli. Na wala huna upendo hata kidogo kwa Mungu. Inaweza kusemwa kuwa hali yako mbele ya Mungu imesambaratika kabisa. Huwezi kushika unachopaswa wala kusema unachopaswa. Huwezi kuweka katika vitendo kile ambacho unapaswa, na huwezi kutekeleza kazi unayopaswa. Huna uaminifu, dhamiri, utii ama azimio unalopasa. Hujavumilia mateso unayopaswa kuwa umevumilia, na huna imani unayopaswa kuwa

nayo. Huna sifa yoyote kabisa; una heshima binafsi ya kuendelea kuishi? Nakuhimiza kwamba ni bora kufunga macho kwa mapumziko ya milele, hivyo kumtoa Mungu katika kujishughulisha nawe na kuvumilia mateso kwa ajili yako. Unaamini katika Mungu lakini bado hujui mapenzi Yake; unakula na kunywa maneno ya Mungu lakini bado huwezi kukidhi mahitaji Yake. Unaamini katika Mungu lakini bado humjui, na kuishi ingawa huna lengo la kujaribu kufikia. Huna maadili na huna madhumuni. Unaishi kama mwanadamu lakini huna dhamiri, uadilifu wowote wala hata uaminifu kidogo. Unafikiriwaje kuwa wanadamu? Unaamini katika Mungu lakini unamdanganya. Zaidi ya hayo, unachukua pesa za Mungu na kula sadaka Yake, na bado, mwishowe, huonyeshi fikira kwa hisia za Mungu ama dhamiri kwa Mungu. Huwezi hata kukidhi mahitaji ya Mungu ya chini zaidi. Kwa hivyo unawezaje kufikiriwa kuwa mwanadamu? Chakula unachokula na hewa unayopumua vimetoka kwa Mungu, unafurahia neema Yake, na bado mwishowe, huna hata ufahamu mdogo wa Mungu. Kinyume na hayo, umekuwa mtu asiye na maana anayempinga Mungu. Si basi wewe ni mnyama asiye bora kuliko mbwa? Kuna mnyama yeyote aliye mkatili kukuliko wewe?

Hao wahubiri na wazee wanaosimama katika mimbari ya juu wakimfundisha mwanadamu ni wapinzani wa Mungu na wako katika muungano na Shetani; wale kati yenu wasiosimama katika mimbari ya juu wakimfundisha mwanadamu hawatakuwa hata wapinzani wakubwa zaidi wa Mungu? Juu ya hayo, huna ushirikiano basi na Shetani? Wale wasioelewa madhumuni ya kazi ya Mungu hawajui kuwa na makubaliano na moyo wa Mungu. Bila shaka, haiwezi kuwa ukweli kwa wale wanaoyaelewa madhumuni ya kazi Yake? Kazi ya Mungu kamwe haina makosa; badala yake, ni kufuatilia kwa mwanadamu kuliko na dosari. Wale waliosawijika wanaompinga Mungu makusudi sio waovu zaidi na mahasidi kuliko hao wahubiri na wazee? Wanaompinga Mungu ni wengi, na miongoni mwa wanadamu hao wengi, kuna aina mbalimbali ya upinzani dhidi ya Mungu. Kwa kuwa kuna kila aina ya waumini, hivyo pia kuna kila aina ya wale wanaompinga Mungu kila tofauti na mwingine. Hakuna mmoja kati ya wale wasiotambua wazi madhumuni ya kazi ya Mungu anayeweza kuokolewa. Bila kujali jinsi mwanadamu anaweza kuwa alimpinga Mungu zamani, mwanadamu ajapo kufahamu madhumuni ya kazi ya Mungu na kujitolea juhudi zake ili kumridhisha Mungu, dhambi zake za awali zitafutiliwa mbali na Mungu. Bora tu mwanadamu anatafuta ukweli na kuuweka ukweli katika vitendo, Mungu hataweka akilini kile ambacho amefanya. Badala yake, ni kwa msingi wa kutenda ukweli kwa mwanadamu ndiyo Mungu anamtetea mwanadamu. Hii ndiyo haki ya Mungu. Kabla ya mwanadamu kumwona Mungu ama kuwa na uzoefu wa kazi Yake, bila kujali jinsi mwanadamu anamtendea Mungu, Haliweki hili akilini. Hata hivyo, mara tu mwanadamu amwonapo Mungu, na kuwa na uzoefu wa kazi Yake, matendo yote na vitendo vyote vya mwanadamu vinaandikwa chini ndani ya “rekodi” na Mungu, kwani mwanadamu amemwona Mungu na kuishi ndani ya

kazi Yake.

Wakati mwanadamu ameona kwa kweli kile Mungu alichio nacho na kile Alichio, aonapo ukuu Wake, na kweli amekuja kujua kazi ya Mungu, na zaidi ya hayo, tabia ya awali ya mwanadamu inabadilika, basi mwanadamu atakuwa ameitupilia mbali kabisa tabia yake ya uasi inayompinga Mungu. Inaweza kusemwa kwamba kila mwanadamu amempinga Mungu wakati mmoja na kila mwanadamu ameasi dhidi ya Mungu. Hata hivyo, kama una akili ya kummtii Mungu mwenye mwili, na kwa hivyo kuuridhisha moyo wa Mungu kwa uaminifu wako, unaweka katika vitendo ukweli unaopaswa, kutekeleza jukumu lako unavyopaswa, na kufuata kanuni unazopaswa, basi wewe ni mtu aliye tayari kutupilia mbali uasi wake kumridhisha Mungu na mtu anayeweza kukamilishwa na Mungu. Iwapo utakataa kutambua makosa yako na huna moyo wa kutubu; ukiendelea katika njia zako za uasi na huna kabisa moyo wa kufanya kazi na Mungu na kumridhisha Mungu, basi mjinga mkaidi kama wewe kwa hakika ataadhibiwa na hatawahi kuwa mmoja wa kukamilishwa na Mungu. Iwapo hivyo, wewe ni adui wa Mungu leo na kesho, na hivyo pia utabaki adui wa Mungu siku ifuatayo; utakuwa milele mpinzani wa Mungu na adui wa Mungu. Mungu atakuachaje? Ni asili ya mwanadamu kumpinga Mungu, lakini mwanadamu hawezi kwa makusudi kutafuta “siri” za kumpinga Mungu kwa sababu kubadili asili yake ni kazi isiyoshindika. Kama hali ni hiyo, basi ni bora uende zako kabla hujachelewa, isiwe kuadibu kwako wakati ujao kukawa kali zaidi, na isiwe asili yako kama ya mnyama ikaibuka na kuwa isiyotawalika mpaka mwili wako unaondolewa na Mungu mwishowe. Unaamini katika Mungu ili ubarikiwe; ikiwa mwishowe, balaa tu ndiyo itakayokupata, hiyo haitakuwa na thamani. Nawahimiza kuunda mpango mwingine; zoezi jingine litakuwa bora kuliko imani yenu kwa Mungu. Hakika kuna mengi kuliko njia hii moja? Hamngeweza kuendelea kuishi vile vile bila kutafuta ukweli? Mbona kuishi katika ukinzani na Mungu kwa namna hii?

Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani II (Novemba 1992 hadi Juni 1993)

Kazi na Kuingia (1)

Tangu watu waanze kuikanyaga njia sahihi ya kumwamini Mungu, kumekuwa na mambo mengi ambayo bado hayajaeleweka vizuri. Bado wapo kwenye mkanganyiko kabisa kuhusu kazi ya Mungu, na kuhusu kiasi gani cha kazi wanapaswa kufanya. Hii, kwa upande mmoja, ni kwa sababu ya kuwa na uelekeo tofauti wa uzoefu wao na mipaka katika uwezo wao wa kupokea; kwa upande mwingine, ni kwa sababu kazi ya Mungu bado haijawaleta watu katika hatua hii. Kwa hiyo, kila mtu anapata utata kuhusu masuala mengi ya kiroho. Sio tu kwamba hamna

uhakika kuhusu kile ambacho mnapaswa kuingia kwacho; bali pia ni wajinga kuhusu kazi ya Mungu. Hili ni zaidi ya suala la hasara kwenu. Ni dosari kubwa iliyopo kwa wale walio katika ulimwengu wa dini. Hii ndiyo sababu kuu ya watu kutomjua Mungu, na hivyo dosari hii ni kasoro ya kawaida miongoni mwa wale wote wanaomtafuta. Hakuna mtu hata mmoja aliyewahi kumjua Mungu, au amekwishawahi kuuona uso Wake halisi. Ni kwa sababu hii ndipo kazi ya Mungu inakuwa ngumu kama kazi ya kuhamisha mlima au kukausha bahari. Ni watu wangapi ambao wameyatao maisha yao kwa ajili ya kazi ya Mungu; ni wangapi wametengwa kwa sababu ya kazi Yake; ni wangapi wameteswa hadi kufa kwa ajili ya kazi Yake; ni wangapi wamelia kwa ajili ya upendo wao kwa Mungu, wamekufa pasipo haki; ni wangapi wamekutana na mateso katili na ya kinyama...? Kwamba majanga haya yatapita—hii sio kwa sababu ya watu kutokuwa na maarifa juu ya Mungu? Inawezekanaje mtu ambaye hamjui Mungu awe na ujasiri wa kusimama mbele Yake? Inawezekanaje mtu anayemwamini Mungu na bado anamtesa awe na ujasiri wa kusimama mbele Yake? Haya si makosa kwa wale walio katika ulimwengu wa kidini pekee, bali ni makosa ya kawaida kwenu na kwao. Watu wanamwamini Mungu bila kumfahamu, ni kwa sababu hii ndio watu hawamheshimu Mungu kwa dhati, na hawamchi Yeye kwa dhati. Hata kuna wale ambao, kwa uwazi na bila haya, kwa majivuno makuu na hali, wanafanya kazi ambayo wanafikiria kichwani wenyewe katika mkondo huu, na wanaifanya kazi iliyoagizwa na Mungu kulingana na matakwa yao wenyewe na tamaa zao zisizo na kadiri. Watu wengi wanafanya ovyoovy, hawamtukuzi Mungu bali wanafuata mapenzi yao wenyewe. Je, hii si mifano mizuri ya mioyo ya watu iliyo na ubinafsi? Je, haya hayaonyeshi dalili nyingi zaidi za udanganyifu walionao watu? Watu wanaweza kuwa wenye akili sana, lakini inawezekanaje karama zao zichukue nafasi ya kazi ya Mungu? Watu wanaweza kujali mzigo wa Mungu, lakini hawawezi kufanya mambo kwa ubinafsi sana. Je, matendo ya watu ni ya kiungu kweli? Je, mtu yeyote anaweza kuhakikishwa kwa namna chanya? Kutoa ushuhuda kuhusu Mungu kurithi utukufu Wake—huyu ni Mungu anayewatenga na kuwainua watu; kwa nafsi yao hawawezi kustahili. Kazi ya Mungu ndio kwanza imeanza, maneno Yake ndio kwanza yameanza kuzungumzwa. Katika hatua hii, watu wanajisikia vizuri katika nafsi yao wenyewe; hii haiwezi kuwa ni kujitafutia fedheha? Wanaelewa kidogo sana. Hata mwanafalsafa mwenye karama ya juu sana, mzungumzaji mzuri kabisa, hawezi kuelezea yote kuhusu uteule wa Mungu—sembuse nyinyi? Ni vyema msijione wakubwa kabisa kupita viwango vya mbinguni, badala yake jioneni kuwa watu wa chini kabisa kuliko watu razini wengine wanaotafuta kumpenda Mungu. Hii ndiyo njia ambayo mnapaswa kutumia kuingia: kujiona wadogo kuliko wengine wote. Kwa nini mjiweke katika viwango vya juu? Kwa nini mjiweke katika heshima hiyo ya juu? Katika safari ndefu ya maisha, mmepega hatua chache tu za kwanza. Mnachokiona ni mkono wa Mungu tu, si mwili mzima wa Mungu. Ni wajibu wenu kuiona kazi ya Mungu zaidi, kugundua zaidi juu ya kile mnachopaswa kuingia ndani, kwa sababu mmebadilika kidogo sana.

Huku Mungu anapomkamilisha mwanadamu na kuigeuza tabia yake, kazi Yake kamwe haikomi, kwa kuwa wanakosa katika njia nyingi sana na wao wamepungukiwa na viwango vilivyowekwa na Yeye. Na kwa hiyo inaweza kusemwa kwamba, machoni pa Mungu, milele mtakuwa watoto waliozaliwa karibuni, wenye sifa muhimu chache sana zinazompendeza Yeye, kwa sababu ninyi ni viumbe tu mikononi mwa Mungu. Kama mtu angeingia katika ridhaa, hangechukiwa sana na Mungu? Kusema kwamba mnaweza kumridhisha Mungu leo ni kuzungumza kutoka kwa mtazamo mdogo wa miili yenu; ikiwa kweli mngelinganishwa dhidi ya Mungu, ninyi daima mngeshindwa uwanjani. Mwili wa mwanadamu haujawahi kupata ushindi. Ni kupitia tu kazi ya Roho Mtakatifu ndio inawezekana kwa mwanadamu kuwa na sifa muhimu za kukomboa. Kwa kweli, kati ya vitu vingi katika uumbaji wa Mungu, mwanadamu ni wa kiwango cha chini sana. Ingawa ni mtawala wa vitu vyote, mwanadamu ni kiumbe pekee ambaye yupo chini ya hila za Shetani, ni kiumbe pekee ambaye anashikwa kwa namna nyingi katika uharibifu wake. Mwanadamu hajawahi kuwa na ukuu juu yake mwenyewe. Watu wengi wanaishi katika uovu wa Shetani, na kuumizwa na dhihaka zake; anawaudhi kwa njia hii hata hapo watakapokuwa wamelemewa kabisa, wakistahimili kila badiliko, kila ugumu katika ulimwengu wa kibinadamu. Baada ya kuwachezea, Shetani huimaliza hatima yao. Na hivyo watu wanapita katika maisha yao yote wakiwa na mkanganyiko, wala hawajawahi kufurahia hata siku moja vitu vizuri ambavyo Mungu amewaandalia, badala yake wanajeruhiwa na Shetani na kuachwa wakiwa wameharibika kabisa. Leo wamekuwa wadhoofu na walegevu sana kiasi kwamba hawana mwelekeo wa kuzingatia kazi ya Mungu. Ikiwa watu hawana mwelekeo wa kuzingatia kazi ya Mungu, uzoefu wao utabakia kuwa vipandevipande na kutokamilika milele, na kuingia kwao kutabakia sehemu tupu milele. Katika Miaka elfu kadhaa tangu Mungu alipokuja duniani, idadi yoyote ya watu wenye mawazo ya kiburi wamekuwa wakitumiwa na Mungu kumfanyia Yeye kazikwa miaka mingi; lakini wale wanaojua kazi Yake ni wachache sana takribani hawapo kabisa. Kwa sababu hii, idadi kubwa ya watu ambao hawajatajwa wanachukua jukumu la kumpinga Mungu wakati huo huo wanapomfanyia kazi, kwa sababu, badala ya kufanya kazi Yake, kimsingi wanafanya kazi ya mwanadamu katika nafasi waliyopewa na Mungu. Je, hii inaweza kuitwa kazi? Wanawezaje kuingia? Mwanadamu amechukua neema ya Mungu na kuizika. Kwa sababu hii, kwa karne nyingi zilizopita wale wanaofanya kazi Yake wana kuingia kwa kiwango kidogo. Hawazungumzi juu ya kuijua kazi ya Mungu kwa sababu wana ufahamu kiasi kidogo wa hekima ya Mungu. Inaweza kusemwa kwamba, ingawa kuna watu wengi wanaomtumikia Mungu, wameshindwa kuona jinsi Alivyoinuliwa, na hii ndiyo sababu watu wamejifanya wao ndio Mungu wa kuabudiwa na watu.

Kwa miaka mingi sana Mungu amebakia sirini katika uumbaji; Ameangalia katika misimu yote ya machipuko na kipupwe nyuma ya umande ufunikao; Ametazama chini kutoka mbingu ya

tatu kwa siku nyingi sana; Ametembea miongoni mwa wanadamu kwa miezi na miaka mingi sana. Amekaa juu ya wanadamu wote Akisubiri kwa utulivu katika vipindi vingi vya baridi. Hajawahi kujionyesha wazi kwa mtu yeyote yule, wala kutoa sauti hata kidogo, Anaondoka bila ishara na kurudi kimyakimya. Nani anaweza kuujua uso wake halisi? Hajawahi kuzungumza na mwanadamu hata mara moja, Hajawahi kuonekana kwa mwanadamu hata mara moja. Ni rahisi kiasi gani kwa watu kufanya kazi iliyoagizwa na Mungu? Wanatambua kidogo tu kwamba kumjua Yeye ni kitu kigumu sana kuliko vitu vyote. Leo Mungu amezungumza na mwanadamu, lakini mwanadamu hajawahi kumfahamu, kwa sababu kuingia kwake katika maisha ni finyu sana na hakuna kina. Kwa mtazamo Wake, watu hawastahili kabisa kuonekana mbele za Mungu. Wana ufahamu kiasi kidogo sana juu ya Mungu na wametanga mbali Naye sana. Aidha, mioyo inayomwamini Mungu ni tatanishi sana, na hawana taswira ya Mungu ndani ya mioyo yao. Na matokeo yake ni, juhudi za Mungu zenye kubeba maumivu, na kazi Yake, kama vipande vya dhahabu vilivyofunikwa mchangani, haviwezi kutoa mwanga. Kwa Mungu, tabia, nia, na mitazamo ya watu hawa ni machukizo sana. Ni dhaifu katika uwezo wao wa kupokea, hawana hisia kiasi cha kufa ganzi, wamejishusha thamani na kuharibika, wametumikishwa kupita kiasi, ni dhaifu wasiokuwa na dhamiri, ni lazima waongozwe kama vile ng'ombe na farasi huongozwa. Kama ilivyo kuingia kwao katika roho, au kuingia katika kazi ya Mungu, hawachukui tahadhari yoyote, hawajizatiti hata kidogo kuteseka kwa ajili ya ukweli. Kwa mtu kama huyu kufanywa mkamilifu na Mungu haitakuwa rahisi. Hivyo ni muhimu kwamba mnapanga kuingia kwenu katika pembe hii—kwamba kupitia kazi yenu na kuingia kwenu ndipo mnakaribia kujua kazi ya Mungu.

Kazi na Kuingia (2)

Kazi na kuingia kwenu ni duni kabisa; mwanadamu hatilii umuhimu jinsi ya kufanya kazi na hata yeye si mzingativu kuhusu kuingia katika uzima. Mwanadamu haoni haya kuwa mafunzo mazuri anayopaswa kuingia ndani; kwa hivyo, katika uzoefu wako, yote ambayo mwanadamu anaona ni njozi. Si mengi yanatakiwa kutoka kwenu kuhusiana na kazi, lakini, kama yule anayetakiwa kukamilishwa na Mungu, mnapaswa kujifunza mafunzo kuhusu kumfanyia Mungu kazi ili hivi punde muweze kuupendeza moyo wa Mungu. Kotekote katika enzi, wale waliofanya kazi wameitwa wafanyakazi au mitume, ambayo inahusu idadi ndogo ya watu waliotumiwa na Mungu. Hata hivyo, kazi Niizungumziayo leo haihusu wafanyakazi au mitume hao pekee; inaelekezwa kwa wote watakaokamilishwa na Mungu. Labda kuna wengi walio na hamu kidogo katika hili, lakini, kwa ajili ya kuingia, ingekuwa bora zaidi kujadili ukweli huu.

Kazi inapozungumziwa, mwanadamu anaamini kwamba kazi ni kusafiri kwenda huku na huko kwa ajili ya Mungu, akihubiri kila sehemu, na kugharimia rasilimali kwa ajili ya Mungu.

Ingawa imani hii ni sahihi, ni ya kuegemea upande mmoja sana; kile ambacho Mungu anamwomba mwanadamu si kusafiri kwenda huku na huko kwa ajili ya Mungu; ni huduma zaidi na kujitoa ndani ya roho. Ndugu wengi hawajawahi kufikiria juu ya kumfanyia Mungu kazi hata baada ya miaka mingi sana ya uzoefu, maana kazi kama mwanadamu anavyoielewa haipatani na ile ambayo Mungu anaitaka. Kwa hiyo, mwanadamu havutiwi kwa namna yoyote ile na kazi ya Mungu, na hii ndiyo sababu kuingia kwa mwanadamu ni kwa kuegemea upande mmoja kabisa. Nyinyi nyote mnapaswa kuingia kwa kumfanyia Mungu kazi, ili muweze kupata uzoefu wa vipengele vyake vyote. Hiki ndicho mnapaswa kuingia ndani. Kazi haimaanishi kutembea huku na huko kwa ajili ya Mungu; maana yake ni iwapo maisha ya mwanadamu na kile ambacho mwanadamu anaishi kwa kudhihirisha ni kwa ajili ya Mungu kufurahia. Kazi inamaanisha mwanadamu kutumia uaminifu alio nao kwa Mungu na maarifa aliyo nayo juu ya Mungu ili kumshuhudia Mungu na kumhudumia mwanadamu. Huu ndio wajibu wa mwanadamu, na yote ambayo mwanadamu anapaswa kutambua. Kwa maneno mengine, kuingia kwenu ni kazi yenu; mnatafuta kuingia wakati wa kazi yenu kwa ajili ya Mungu. Kupitia kazi ya Mungu hakumaanishi tu kwamba unajua jinsi ya kula na kunywa neno Lake; na muhimu zaidi, mnapaswa kuweza kumshuhudia Mungu, kumtumikia Mungu, na kumhudumia na kumkimu mwanadamu. Hii ni kazi, na pia kuingia kwenu; hiki ndicho kila mwanadamu anapaswa kukitimiza. Kuna watu wengi ambao wanatilia mkazo tu katika kusafiri huku na huko kwa ajili ya Mungu, na kuhubiri kila sehemu, lakini hawazingatii uzoefu wao binafsi na kupuuza kuingia kwao katika maisha ya kiroho. Hiki ndicho kinasababisha wale wanaomtumikia Mungu kuwa watu wanaompinga Mungu. Kwa miaka mingi sana, wale wanaomtumikia Mungu na kumhudumia mwanadamu wanaona kufanya kazi na kuhubiri kuwa ndio kuingia, na hakuna anayechukulia uzoefu wake binafsi wa kiroho kuwa kuingia muhimu. Badala yake, wanatumia nuru ya kazi ya Roho Mtakatifu kuwafundisha wengine. Wanapohubiri, wanakuwa na mzigo mkubwa sana na wanapokea kazi ya Roho Mtakatifu, na kupitia hili wanatoa sauti ya Roho Mtakatifu. Wakati huo, wale wanaofanya kazi wanahisi kuridhika kana kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ni uzoefu wao binafsi wa kiroho; wanahisi kwamba maneno yote wanayoyazungumza wakati huo ni ya yao wenyewe, na pia kana kwamba uzoefu wao si wazi kama walivyoieleza. Kuongezea, wao hawana fununu ya nini cha kusema kabla ya kunena, lakini Roho Mtakatifu anapofanya kazi ndani yao, wao huwa na mtiririko wa maneno usioisha na usiosita. Baada ya kuwa umehubiri kwa namna hiyo, unahisi kwamba kimo chako halisi sio kidogo kama ulivyoamini. Baada ya Roho Mtakatifu kufanya kazi ndani yako kwa namna ile ile mara kadhaa, basi unaamini kwamba tayari una kimo na unaamini kimakosa kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ni kuingia kwako na asili yako mwenyewe. Unapopitia uzoefu huu kwa mfululizo, unakuwa mzembe kuhusu kuingia kwako. Halafu unakuwa mvivu bila kujua, na kutozingatia kabisa kuingia kwako mwenyewe. Kwa hiyo, unapowahudumia wengine, unapaswa kutofautisha

waziwazi kati ya kimo chako na kazi ya Roho Mtakatifu. Hii itasaidia zaidi kuingia kwako na kunufaisha zaidi uzoefu wako. Mwanadamu akidhani kazi ya Roho Mtakatifu ni uzoefu wake binafsi ndio mwanzo wa upotovu. Hivyo, kazi yoyote mnayoifanya, mnapaswa kuzingatia kuingia kwenu kama somo muhimu.

Mtu anafanya kazi ili kutimiza mapenzi ya Mungu, kuwaleta wale wote wanaoutafuta moyo wa Mungu mbele Yake, kumleta mwanadamu kwa Mungu, na kuitambulisha kazi ya Roho Mtakatifu na uongozi wa Mungu kwa mwanadamu, kwa kufanya hivyo atakuwa anayakamilisha matunda ya kazi ya Mungu. Kwa sababu hii, ni muhimu kuelewa kiini cha kufanya kazi. Kama mtu anayetumiwa na Mungu, watu wote wanafaa kumfanyia kazi Mungu, yaani, wote wana fursa ya kutumiwa na Roho Mtakatifu. Hata hivyo kuna hoja moja mnayopaswa kuielewa: Mwanadamu anapofanya kazi iliyoagizwa na Mungu, mwanadamu anakuwa amepewa fursa ya kutumiwa na Mungu, lakini kile kinachosemwa na kujulikana na mwanadamu sio kimo cha mwanadamu kabisa. Mnaweza tu kujua vizuri kasoro zako katika kazi yenu, na kupokea nuru kubwa kutoka kwa Roho Mtakatifu, kwa kufanya hivyo mtakuwa mnaweza kupata kuingia kuzuri katika kazi yenu. Ikiwa mwanadamu anachukulia uongozi wa Mungu kuwa ni kuingia kwake mwenyewe na kile kilichomo ndani ya mwanadamu, hakuna uwezo wa mwanadamu kuongezeka kimo. Roho Mtakatifu humpatia mwanadamu nuru anapokuwa katika hali ya kawaida; katika nyakati kama hizo, mara nyingi mwanadamu anadhani nuru anayopokea ni kimo chake mwenyewe katika uhalisi, maana Roho Mtakatifu huangazia katika njia ya kawaida: kwa kutumia kile ambacho ni cha asili kwa mwanadamu. Mwanadamu anapofanya kazi na kuzungumza, au wakati mwanadamu anapofanya maombi katika shughuli zake za kiroho, ndipo ukweli utawekwa wazi kwao. Hata hivyo, katika uhalisi, kile ambacho mwanadamu anakiona ni nuru tu iliyoangaziwa na Roho Mtakatifu (kwa kawaida, hii inahusiana na ushirikiano kutoka kwa mwanadamu) na sio kimo halisi cha mwanadamu. Baada ya kipindi cha kupitia ambapo mwanadamu anakabiliwa na shida na majaribu fulani, kimo cha kweli cha mwanadamu hudhihirika katika mazingira kama hayo. Ni katika muda huo ndipo mwanadamu anagundua kwamba kimo cha mwanadamu sio kikubwa hivyo, na ubinafsi, fikira zake mwenyewe, na tamaa za mwanadamu vyote huibuka. Ni baada tu ya mizunguko kadhaa ya uzoefu kama huo ndipo wengi wa jinsi hiyo ambao wameamshwa ndani ya roho zao watatambua kwamba haukuwa uhalisi wao hapo nyuma, bali ni mwangaza wa muda tu kutoka kwa Roho Mtakatifu, na mwanadamu alipokea nuru tu. Roho Mtakatifu anapompa mwanadamu nuru ili aelewe ukweli, mara nyingi inakuwa katika namna ya wazi na tofauti, bila kueleza jinsi ambavyo mambo yalitokea au kule yanakoenda. Yaani, Hayajumuishi matatizo ya mwanadamu katika ufunuo huu, na badala yake Anatoa ufunuo moja kwa moja. Mwanadamu anapokabiliana na matatizo katika kuingia, basi mwanadamu anaijumuisha nuru ya Roho Mtakatifu, na huu unakuwa uzoefu halisi

wa mwanadamu. Kwa mfano, dada ambaye hajaolewa ananena hivi wakati wa ushirika: “Hatutafuti sifa kuu na utajiri au kutamani furaha ya upendo kati ya mume na mke; sisi hutafuta tu kuutoa moyo wa utakatifu na umakini kwa Mungu.” Anaendelea kusema: “Mara tu watu wanapoolewa au kuoa, kuna mengi ambayo huwazonga, na moyo wao wa kumpenda Mungu si halisi tena. Mioyo yao daima hushughulishwa na familia zao na wake au waume zao, na kwa hiyo mioyo yao huwa yenye utata zaidi....” Anapozungumza, ni kana kwamba maneno ayanenayo ni yale anayofikiria moyoni mwake; maneno yake ni ya kuvuma na yenye nguvu, kana kwamba yote anenayo yanatoka ndani kabisa ya moyo wake. Anatamani angejitolea kabisa kwa Mungu na anatumaini kwamba ndugu kama yeye wanashiriki azimio lilo hilo. Inaweza kusemwa kwamba azimio lako na hisia ya kulisimuliwa wakati huu yote hutoka kwa kazi ya Roho Mtakatifu. Wakati ambapo mbinu ya kazi ya Mungu hubadilika, umekua miaka michache kwa umri; unaona kwamba wanafunzi wenzako wote na marafiki wa umri wako wana waume, au unasikia kwamba baada ya fulani na fulani kuolewa, mume wake alimpeleka mjini kuishi na akapata kazi huko. Unapomwona, moyo wako huanza kuona wivu. Unaona kwamba amejaa uzuri na mkao toka utosini hadi wayoni; anapozungumza, ana wepesi wa kiulimwengu, hana tena ushamba wa mashambani kumhusu. Hili husisimua hisia ndani yako. Wewe, baada ya kugharimia rasilimali kwa ajili ya Mungu wakati huu wote, huna familia au kazi, na umevumilia kushughulikiwa kwingi; kitambo sana, uliingia katika umri wa makamo, na ujana wako ukaponyoka kimya, kana kwamba umepumbaa. Umefika umbali huu wote mpaka siku hii, lakini hujui ni wapi utatulia. Ni wakati huo ndipo unakuwa katika kimbunga cha mawazo, kana kwamba wewe ni mwenye wazimu. Ukiwa mpweke na usiyeweza kulala fofofu, ukiona ugumu kupata usingizi usiku wote, wewe, kabla hujajua, unaanza kufikiri juu ya azimio lako na nadhiri zako za dhati kwa Mungu, na kwa nini, hata hivyo, umeanguka katika hali ya kuhuzunisha kama hiyo? Punde si punde, machozi ya kimyakimya yanakutoka na unahisi uchungu kabisa. Unakuja mbele za Mungu kuomba na unaanza kufikiria juu ya urafiki wa karibu sana na kukaribiana kwa kutotengana kwa wakati wa siku zako za furaha na Mungu. Onyesho baada ya onyesho linaonekana mbele ya macho yako, na nadhiri uliyoweka siku hiyo inabaki mara tena akilini mwako, “Je, Mungu si mwandani wangu wa pekee?” Kufikia wakati huo, unamamia: “Mungu! Mungu mpenzi! Nimeshakupa Wewe moyo wangu wote. Ningependa kuahidiwa Kwako milele, na nitakupenda Wewe bila kubadilika maisha yangu yote....” Ni wakati ambao unang’ang’ana tu katika mateso hayo ya kuzidi kiasi ndiyo unahisi kweli jinsi Mungu alivyo wa kupendeza, na wakati huo tu ndipo unatambua kwa dhahiri: Nilijitolea kabisa kwa Mungu kitambo sana. Baada ya pigo kama hilo, unakuwa na uzoefu zaidi katika jambo hili na kuona kwamba kazi ya Roho Mtakatifu wakati huo si miliki ya mwanadamu. Katika uzoefu wako baadaye, wewe hauzuiwi tena katika kuingia huku; ni kana kwamba makovu yako yamefaidisha sana kuingia kwako. Wakati wowote unapokabiliwa na hali kama hizo, mara moja utakumbuka machozi yako tangu

siku hiyo, kana kwamba unaunganishwa tena na Mungu. Una woga siku zote wa kuuvunja uhusiano wako na Mungu tena na kuharibu penzi la hisia (uhusiano wa kawaida) kati yako na Mungu. Hii ni kazi yako na kuingia kwako. Kwa hiyo, mnapoipokea kazi ya Roho Mtakatifu, mnapaswa kujikita zaidi katika kuingia kwenu, na wakati huo huo, kuona kipi ni kazi ya Roho Mtakatifu na kipi ni kuingia kwenu, vilevile kujumuisha kazi ya Roho Mtakatifu katika kuingia kwenu, ili kwamba muweze kukalishwa Naye vizuri na kuruhusu hulka ya kazi ya Roho Mtakatifu kuletwa pamoja ndani yenu. Wakati mnapitia uzoefu wenu wa kazi ya Roho Mtakatifu, mnamjua Roho Mtakatifu, vilevile nyinyi wenyewe, na katikati ya mateso makali, mnajenga uhusiano wa kawaida pamoja na Mungu, na uhusiano baina yenu na Mungu unakuwa wa karibu siku kwa siku. Baada ya michakato mingi ya kupogolewa na kusafishwa, mnakuza upendo wa kweli kwa Mungu. Hii ndiyo sababu mnapaswa kutambua kwamba mateso, mapigo, na dhiki havitishi; kinachoogopesha ni kuwa na kazi ya Roho Mtakatifu tu lakini sio kuingia kwenu. Siku inapofika kwamba kazi ya Mungu imemalizika, mtakuwa mmefanya kazi bure; ingawa mmepitia uzoefu wa kazi ya Mungu, hamtakuwa mmemjua Roho Mtakatifu au kuwa na kuingia kwenu wenyewe. Nuru anayopewa mwanadamu na Roho Mtakatifu si ya kudumisha hisia za mwanadamu; ni kufungua njia kwa ajili ya kuingia kwa mwanadamu, vilevile kumruhusu mwanadamu kumjua Roho Mtakatifu, na kuanzia hapo anakuza moyo wa uchaji na ibada kwa Mungu.

Kazi na Kuingia (3)

Mungu amewaaminia wanadamu vitu vingi sana na Amezungumza bila kikomo juu ya kuingia kwao. Lakini kwa sababu ubora wa tabia ya watu ni duni mno, maneno mengi ya Mungu yameshindwa kuanza kustawi. Kuna sababu mbalimbali za huu ubora duni wa tabia, kama vile uharibifu wa mawazo na maadili ya binadamu, na kutokuwa na malezi mazuri; imani za usihiri zilizojaa moyoni mwa mwanadamu; mitindo ya maisha iliyopotoka ambayo imeweka maovu mengi katika sehemu ya ndani kabisa ya moyo wa mwanadamu; ufahamu wa juujuu wa utamaduni, na takribani asilimia tisini na nane ya watu ambao hawana elimu ya utamaduni na, aidha, watu wachache sana wanaopata viwango vya juu vya elimu ya utamaduni. Kwa hivyo, kimsingi watu hawajui ni nini maana ya Mungu au Roho, bali wana taswira hafifu ya Mungu na isiyoeleweka vizuri kama iliyopatikana kutoka kwa imani ya usihiri. Ushawishi wenye madhara ambao maelfu ya miaka ya “roho wa juu sana wa utaifa” umeacha ndani kabisa ya moyo wa mwanadamu pamoja na fikira za kikabaila ambazo watu wamefungwa nazo na kutiwa minyororo, bila uhuru wowote, na kusababisha watu kutokuwa na hamasa au ustahimilivu, hawana shauku ya kusonga mbele, lakini badala yake wanakuwa baridi na kurudi nyuma, wakiwa na akili ya utumwa ambayo ina nguvu sana, na kadhalika—sababu hizi zimetengeneza taswira chafu na mbaya kwa mitazamo ya njozi, mawazo, maadili, na tabia ya binadamu.

Inaonekana, wanadamu wanaishi katika dunia ya giza la kutisha, na hakuna anayetafuta kusonga mbele miongoni mwao, hakuna anayefikiria kwenda katika ulimwengu ulio bora, badala yake, wanaridhika na waliyo nayo maishani, kutumia siku zao kuzaa na kuwalea watoto, wakikazana, wakitoka jasho, wakifanya kazi zao, wakiwa na njozi ya kuwa na familia ya raha na yenye furaha, ya upendo wa ndoa, ya watoto wenye upendo, ya maisha yenye furaha katika miaka yao ya uzeeni wanapoishi kwa kudhihirisha maisha yao kwa amani. ... Kwa makumi, maelfu, makumi ya maelfu ya miaka hadi sasa, watu wamekuwa wakipoteza muda wao kwa njia hii, hakuna anayetengeneza maisha makamilifu, wanapigana tu wenyewe kwa wenyewe katika ulimwengu huu wa giza, wakipambana kupata umaarufu na utajiri, na kufanyiana njama wao kwa wao. Nani amewahi kutafuta mapenzi ya Mungu? Kuna mtu yeyote aliyewahi kutilia maanani kazi ya Mungu? Sehemu hizi zote za binadamu zinazomilikiwa na ushawishi wa giza zimekuwa asili ya mwanadamu tangu zamani, kwa hiyo ni vigumu sana kutekeleza kazi ya Mungu na hata watu hawana moyo wa kuzingatia kile ambacho Mungu amewaaminia leo. Vyovyote vile, Ninaamini kwamba watu hawatajali Ninapotamka maneno haya kwa vile kile Ninachokisema ni historia ya maelfu ya miaka. Kuzungumza juu ya historia kuna maana ya ukweli na, zaidi ya hayo, kashfa zinazojulikana kwa wote, sasa kuna maana gani kuzungumza kitu ambacho ni kinyume na ukweli? Lakini pia Naamini kwamba watu wenye akili, wanapoona maneno haya, wataamka na kujitahidi kwa ajili ya kuendelea mbele. Mungu hutumaini kwamba wanadamu wanaweza kuishi na kufanya kazi kwa amani na kuridhika huku wakati ule ule wakiweza kumpenda Mungu. Ni mapenzi ya Mungu kwamba binadamu wote waweze kuingia katika raha; zaidi ya hili, kuijaza nchi yote na utukufu wa Mungu ni shauku kubwa ya Mungu. Ni aibu tu kwamba wanadamu husalia katika hali ya kusahauliwa kabisa na wasiotambua mambo, waliopotoshwa vibaya sana na Shetani hivi kwamba leo hawafanani tena na binadamu. Kwa hiyo mawazo ya binadamu, uadilifu na elimu huunda kiungo muhimu, pamoja na mafunzo katika kujua kusoma na kuandika utamaduni yakiunda kiungo cha pili, bora zaidi ya kuinua ubora wa tabia wa utamaduni wa binadamu na kubadilisha mtazamo wao wa kiroho.

Kwa kweli, mahitaji ya Mungu kwa binadamu si mengi, lakini kwa sababu pengo kati ya uhodari wa watu na kiwango anachohitaji Mungu ni kikubwa sana, watu wengi sana hutazama tu upande wa matakwa ya Mungu lakini hukosa uwezo wa kuyatimiza. Kipaji cha watu cha asili, pamoja na kile wanachojiandaa nacho baada ya kuzaliwa, kiko mbali sana na kutimiza matakwa ya Mungu. Bali kutambua tu wazo hili si suluhisho la hakika kufanikiwa. Maji ya mbali hayawezi kukata kiu ya sasa hivi. Hata watu wakijifahamu kuwa duni kuliko vumbi, kama hawana azimio la kuuridhisha moyo wa Mungu, sembuse kuifuata njia iliyoko mbele ili kutimiza matakwa ya Mungu, basi maarifa ya aina hiyo yana thamani gani? Je, si kama kuchota maji na chungio—juhuri isiyo na maana? Kiini cha kile Nisemacho kinahusu kuingia; hiyo ndiyo mada

kuu.

Wakati wa kuingia kwa mwanadamu, maisha huwa ya kuchosha daima, yaliyojaa sifa za lazima zisizobadilika za maisha ya kiroho, kama vile kufanya maombi, kula na kunywa maneno ya Mungu kiasi, au kufanya mikusanyiko, ili watu wahisi daima kwamba kumwamini Mungu hakuleti raha kuu. Shughuli za kiroho kama hizo kila mara hutekelezwa kwa msingi wa tabia ya asili ya binadamu, ambao wamepotoshwa na Shetani. Ingawa wakati mwingine watu wanaweza kupokea nuru ya Roho Mtakatifu, kufikiri kwao kwa asili, tabia, mitindo ya maisha na mienendo bado imekita mizizi, na kwa hiyo asili yao husalia isiyobadilika. Shughuli za kishirikina ambazo watu wanashughulika nazo ndizo Mungu anazichukia sana, lakini watu wengi bado hawawezi kuachana nazo, wakifikiri kwamba shughuli hizi za kishirikina zimeamriwa na Mungu, na hata leo bado hawajaziacha kabisa. Mambo kama mipango ambayo vijana hufanya kwa ajili ya sherehe za arusi au mahari, zawadi za pesa, dhifa, na maneno mengine na virai vinavyohusiana na matukio ya sherehe; maneno ya zamani ambayo yamerithishwa; shughuli zote za kishirikina zisizokuwa na maana zinazofanywa kwa niaba ya wafu na taratibu za mazishi; yote haya yanachukiwa sana na Mungu. Hata siku ya ibada (ikiwemo Sabato, kama inavyoadhimishwa na ulimwengu wa dini) inachukiwa naye; mahusiano ya kijamii na mawasiliano ya kidunia kati ya mwanamme na mwanamme pia yanachukiwa na kukataliwa zaidi na Mungu. Hata Sikukuu ya Machipuko na Siku ya Krismasi, ambazo zinajulikana kwa kila mtu, haziamriwi na Mungu, sembuse wanasesere na mapambo ya sherehe za siku kuu hizi kama vile mashairi, mafataki, kandili, Komunyo, zawadi za Krismasi na sherehe za Krismasi—je, sio sanamu katika akili za wanadamu? Kumega mkate siku ya Sabato, mvinyo, na kitani nyembamba navyo ni sanamu zaidi. Siku zote za sherehe za kijadi ambazo ni maarufu sana nchini China, kama vile Siku ya kuinua Vichwa vya Joka, Sikukuu ya Mashua ya Joka, Sikukuu ya Majira ya Kati ya Kupukutika, Sikukuu ya Laba, na Siku ya Mwaka Mpya, na sikukuu zisizothibitika katika ulimwengu wa kidini, kama vile Pasaka, Siku ya Ubatizo, na Siku ya Krismasi, zote hizi zimepangwa na kurithishwa kwa watu wengi tangu zama za kale hadi leo. Ni uwezo mkubwa wa fikra za binadamu na dhana bunifu ambazo zimewaruhusu kurithishwa hadi leo. Zinaonekana kuwa hazina kasoro, lakini kwa kweli ni hila ambazo Shetani alifanya kwa binadamu. Kadri Shetani wanavyoishi katika eneo fulani, na kadri eneo hilo lilivyo nyuma kimaendeleo na kutofaa, ndivyo desturi zake za kikabaila zinakuwa nyingi zaidi. Vitu hivi vinawafunga watu kwa nguvu, bila kutoa nafasi kwa ajili ya maendeleo. Sikukuu nyingi katika ulimwengu wa kidini zinaonekana kuonyesha ubunifu mkubwa na zinaonekana kujenga daraja kwa kazi ya Mungu, lakini kweli ni vifungo visivyoshikika ambavyo Shetani hutumia kuwafunga watu ili wasije kumjua Mungu—hizi zote ni hila za ujanja za Shetani. Kwa kweli, hatua ya kazi ya Mungu inapomalizika, tayari Amekwishaharibu zana na mtindo wa wakati huo, bila kuacha

alama yoyote. Hata hivyo, “waumini wasalihina” bado wanaabudu vitu hivyo vya kushikika; wakati huo huo wanaacha kile Alichu nacho Mungu, bila hata kukichunguza zaidi, wakionekana wamejawa na upendo wa Mungu lakini kwa uhalisi walimtoa ndani ya nyumba zamani sana na kumweka Shetani mezani kwa ajili ya kumwabudu. Sanamu ya Yesu, Msalaba, Maria, Ubatizo wa Yesu na Karamu ya Mwisho—watu wanavichukulia hivi kama Bwana wa Mbinguni, wanaviabudu wakati wote wakilia kwa sauti kwa kurudiarudia “Bwana, Baba wa Mbinguni.” Je, huu wote sio utani? Hadi leo, misemo mingi ya kimapokeo kama hiyo iliyorithishwa miongoni mwa wanadamu ni chukizo kwa Mungu; inazuia kabisa njia ya kuendelea mbele kwa Mungu na, zaidi ya hayo, inasababisha vipingamizi vikubwa kwa kuingia kwa mwanadamu. Mbali na kiwango ambacho Shetani amemharibu mwanadamu, sheria ya Witness Lee, uzoefu wa Lawrence, uchunguzi wa Watchman Nee, na kazi ya Paulo, haya yote yameuteka moyo wa mwanadamu. Mungu hana namna ya kufanya kazi kwa wanadamu, kwa sababu ndani yao kuna ubinafsi mwingi, sheria, kanuni, taratibu na mifumo, na vitu kama hivi; vitu hivi, ukiongezea vitendo vya watu vya imani za kishirikina, vimewakamata na kuwaharibu wanadamu. Ni kana kwamba mawazo ya watu ni filamu ya ajabu ya kichimbakazi katika rangi kamili, ikiwa na watu wa ajabu wakiendesha mawingu, ya kubuni sana kiasi cha kuwastaajabisha watu, ikiwaacha watu wametunduwazwa na kupigwa butwaa. Kusema kweli, kazi ambayo Mungu huja kufanya leo ni hasa kushughulikia na kuondoa sifa za ushirikina za binadamu na kugeuza kabisa mtazamo wao wa akili. Kazi ya Mungu haijadumu hadi leo kwa sababu ya urithi ambao umepitishwa kwa vizazi na binadamu; ni kazi kama ilivyoanzishwa na Yeye binafsi na kukamilishwa na Yeye, bila haja yoyote ya kuurithi urithi wa mwanadamu fulani mkuu wa kiroho, au kurithi kazi yoyote ya asili ya uwakilishi iliyofanywa na Mungu katika enzi nyingine fulani. Binadamu hawahitaji kujishughulisha na jambo lolote kati ya haya. Mungu ana mtindo mwingine leo wa kuzungumza na wa kufanya kazi, kwa hiyo mbona binadamu wajisumbue? Kama wanadamu watatembea njia ya leo katika mkondo wa sasa huku wakiendeleza urithi wa “babu” zao, hawatafikia hatima yao. Mungu huhisi kinyaa sana kwa hali hii hasa ya tabia ya mwanadamu, jinsi Anavyoichukia mno miaka, miezi na siku za ulimwengu wa binadamu.

Njia bora zaidi ya kubadilisha tabia ya mwanadamu ni kuondoa vitu hivi vyenye sumu kubwa katika mioyo ya wanadamu, kuwaruhusu watu kuanza kubadilisha fikira na maadili yao. Kwanza kabisa, watu wanatakiwa kuona waziwazi kwamba kaida zote hizi za kidini, shughuli za kidini, miaka na miezi, na sikukuu zote ni za kumchukiza Mungu. Wanatakiwa kuwa huru kutoka kwa vifungo hivi vya fikira za kishirikina na kuondoa kila alama ya kishirikina iliyozama kabisa ndani. Mambo haya yote ni sehemu ya kuingia kwa mwanadamu. Mnatakiwa kuelewa kwa nini Mungu huwatoa watu katika ulimwengu usiokuwa na dini, na pia kwa nini Huwatoa katika desturi na kanuni. Hili ndilo lango la kuingia kwenu, na ingawa mambo haya hayahusiani na

uzoefu wenu wa kiroho, hivi ndivyo vizuizi vikubwa vinavyozuia kuingia kwenu, vinavyowazuia kumjua Mungu. Vinatengeza wavu unaowakamata watu. Watu wengi husoma Biblia sana na wanaweza hata kukariri mafungu mengi kutoka katika Biblia. Katika kuingia kwao leo, watu bila kujua wanaitumia Biblia kupima kazi ya Mungu, kana kwamba msingi wa hatua hii katika kazi ya Mungu ni Biblia na chanzo chake ni Biblia. Kazi ya Mungu inapokuwa sambamba na Biblia, watu huiunga mkono kazi ya Mungu kwa nguvu zote na kumwangalia Mungu kwa taadhima mpya; kazi ya Mungu inapokuwa haifanani na Biblia, watu huwa na dukuduku sana kiasi cha kuanza kutokwa jasho, wakitafuta ndani yake msingi wa kazi ya Mungu; kama kazi ya Mungu haikutajwa katika Biblia, watu watampuuza Mungu. Inaweza kusemwa kwamba, watu wengi wanaikubali kwa hadhari sana, wanatii kwa kusita, na hawajali kuhusu kuijua kazi ya Mungu; na kuhusu mambo yaliyopita, wanashikilia nusu moja na kuacha nusu nyingine. Je, huku kunaweza kuitwa kuingia? Kushikilia vitabu vya wengine kama hazina, na kuvichukulia kama ufunguo wa dhahabu wa kufungua lango la ufalme, watu hawaonyeshi kuvutiwa na matakwa ya Mungu ya leo. Aidha, “wataalamu wengi wenye akili” katika mkono wao wa kushoto wanashikilia maneno ya Mungu, huku katika mkono wa kulia wanashikilia “kazi kuu” za wengine, kana kwamba wanataka kupata msingi wa maneno ya Mungu ya leo ndani ya kazi hizi kuu ili kuthibitisha kwa ukamilifu kwamba maneno ya Mungu ni sahihi, na hata wanatoa ufafanuzi kwa wengine kwa kuunganisha na kazi kuu, kana kwamba walikuwa wanafanya kazi. Kusema kweli, kuna “watafiti wa kisayansi” wengi miongoni mwa wanadamu ambao hawajawahi heshimu mafanikio makubwa ya kisayansi ya leo, mafanikio ya kisayansi ambayo hayana kigezo (yaani, kazi ya Mungu, maneno ya Mungu, na njia ya kuingia uzimani), hivyo watu wote “wanajitegemea,” “wakihubiri” mbali sana wakitegemea sana ufasaha wao, wakiringia “jina zuri la Mungu.” Wakati huo huo, kuingia kwao kuko hatarini na umbali wa matakwa ya Mungu unaonekana kuwa mbali sana jinsi uumbaji ulivyo mbali na wakati huu. Ni rahisi kiasi gani kufanya kazi ya Mungu? Inaonekana kwamba watu wamekwishaamua kuacha nusu yao kwa mambo ya zamani na kuleta nusu yao kwa wakati wa leo, kuwasilisha nusu kwa Shetani na kukabidhi nusu kwa Mungu, kana kwamba hii ndiyo njia ya kutuliza dhamiri yao na kuweza kuwa na hisia ya utulivu fulani. Mioyo ya watu inadhuru sana kwa siri, wanaogopa sio tu kupoteza kesho bali pia wanahofia kupoteza jana, wanaogopa sana kumkosea Shetani na kumkosea Mungu wa leo, Anayeonekana kuwa na bado kutokuwa. Kwa sababu watu wameshindwa kukuza vizuri fikira na maadili yao, wanakosa utambuzi kabisa, na kimsingi hawajui kama kazi ya leo ni ile ya Mungu au siyo. Pengine ni kwa sababu fikra za kishirikina za watu zimekita mizizi sana kiasi kwamba ushirikina na ukweli, Mungu na sanamu, vimewekwa katika kundi moja; wala hawajali kuvibainisha vitu hivi, na inaonekana kama wametesa bongo zao lakini bado mambo hayo hayajawa wazi. Na hiyo ndio maana wanadamu wamesimama katika njia zao na hawasongi mbele tena. Haya yote yanatokea kwa sababu watu hawana elimu

ya itikadi ambayo ni sahihi, kitu ambacho husababisha ugumu katika kuingia kwao. Na matokeo yake, watu wanapoteza mvuto kabisa katika kazi ya Mungu wa kweli, bali wanashikilia kwa kung'ang'ania^[1] kazi ya mwanadamu (kama vile watu wanaotazamwa kuwa ni watu wakubwa) kana kwamba wamepigwa chapa nayo. Je, hizi si mada mpya kabisa ambazo wanadamu wanapaswa kuingia ndani?

Tanbihi:

1. “Wanashikilia kwa kung'ang'ania” inatumiwa kwa dhihaka. Kirai hiki kinaonyesha kwamba watu ni wakaidi na wasiodhibitiwa kwa urahisi, wakishikilia vitu vilivyopitwa na wakati na wasiopenda kuviachilia.

Kazi na Kuingia (4)

Ikiwa mwanadamu anaweza kuingia kabisa kulingana na kazi ya Roho Mtakatifu, maisha yake yatachipuka haraka kama mmea wa mwanzi baada ya mvua ya majira ya kuchipua. Kwa kuangalia kimo cha sasa wa watu wengi, hakuna mtu hata mmoja anayetilia mkazo umuhimu wa uzima. Badala yake, watu wanaweka umuhimu katika baadhi ya mambo ya juujuu yasiyokuwa na umuhimu. Au wanakimbia huku na kule na kufanya kazi bila malengo na ovyoovyoyila mwelekeo, hawajui waende njia gani na zaidi kwa ajili ya nani. “Wanajificha wenyewe katika unyenyekevu.” Ukweli ni kwamba, ni wachache miongoni mwenu mnaojua makusudi ya Mungu kuhusu siku za mwisho. Ni wachache sana miongoni mwenu wanaojua nyayo za Mungu, lakini hata mbaya zaidi, hakuna anayejua utimilifu wa mwisho wa Mungu utakavyokuwa. Halafu kila mtu, kwa utashi tupu, anakubali kufundishwa nidhamu na kushughulikiwa na wengine, kana kwamba wanapiga misuli na kujitayarisha kwa vita^[1] wakiwa wakisubiri wakati wao wa ushindi. Sitatoa maoni yoyote juu ya “maajabu” haya miongoni mwa watu, lakini kuna hoja moja ambayo wote mnapaswa kuielewa. Kwa sasa watu wengi wanakua wakielekea katika hali isiyo ya kawaida,^[2] na kwa hatua zao za kuingia ndani wanaandamana kuelekea mwisho kabisa.^[3] Kunaweza kuwa na watu wengi wanaofikiri kwamba ni jamii nje ya ulimwengu wa mwanadamu ambao mwanadamu anatamani, akiuamini kuwa ufalmewa uhuru, lakini kwa hakika sivyo ilivyo. Mtu anaweza kusema kwamba watu wamekwishapotoka tayari. Lakini bila kujali kile watu wanachokifanya, bado Nahitaji kuzungumza juu ya kile ambacho mwanadamu anapaswa kuingia ndani. Ustahilifu na kasoro za umati sio mada ya msingi ya majadiliano haya. Natumaini kwamba ndugu wote wataweza kupokea maneno Yangu kabisa na kwa usahihi na sio kuelewa visivyo nia Yangu.

Mungu Amekuwa mwili katika nchi ya China, ambayo wenyeji wa Hong Kong na Taiwan wanaiita bara. Mungu Alipokuja kutoka juu na kuja duniani, hakuna mtu mbinguni wala duniani aliyejua, maana hii ndiyo maana ya kweli ya Mungu kurudi kwa namna ya siri. Amekuwa katika mwili Akifanya kazi na kuishi kwa muda mrefu, bado hakuna mtu yeyote aliyejua. Hata leo hii,

hakuna mtu anayetambua. Pengine hiki kitabakia kuwa kitendawili cha milele. Mungu kuja katika mwili wakati huu sio kitu ambacho mtu yeyote anaweza kujua. Haijalishi ni kwa kiwango kikubwa kiasi gani Roho Mtakatifu Anafanya kazi, siku zote Mungu yupo katika hali ya utulivu, kamwe Hajiachilii mbali. Mtu anaweza kusema kwamba inaonekana kama hatua hii ya kazi Yake inafanyika mbinguni. Ingawa ipo wazi kabisa kwa kila mtu, hakuna anayeitambua. Mungu Atakapomaliza hatua hii ya kazi Yake, binadamu wote wataachana na mtazamo wao wa kawaida,^[4] na kuamka kutoka katika ndoto yao ndefu. Nakumbuka Mungu Alishawahi kusema, “Kuja katika mwili wakati huu ni sawa na kuanguka katika tundu la duma.” Hii ina maana kwamba kwa sababu awamu hii ya kazi ya Mungu imemfanya Mungu kuja katika Mwili na kuzaliwa katika makazi ya joka kuu jekundu, hata kuliko awali, Anakumbwa na hatari kubwa kwa kuja duniani wakati huu. Anachokabiliana nacho ni visu na bunduki na kumbi za starehe; Anavyokabiliana navyo ni vishawishi; Anaokutana nao ni umati wa watu wenye sura za wauaji. Ana hatari ya kuuawa wakati wowote. Mungu Alikuwa na ghadhabu. Hata hivyo, Alikuwa ili Aweze kufanya kazi ya utakasaji, ikiwa na maana kwamba kufanya sehemu ya pili ya kazi Yake inayoendelea baada ya kazi ya wokovu. Kwa ajili ya hatua hii ya kazi Yake, Mungu Amejitolea mawazo na uangalizi wa hali ya juu kabisa na Anatumia njia yoyote inayoweza kufikiriwa ili kuepuka mashambulio ya majaribu, Anajificha katika unyenyekevu Wake na kamwe haringii utambulisho Wake. Katika kumwokoa mwanadamu msalabani, Yesu Alikuwa Anakamilisha tu kazi ya wokovu; Alikuwa hafanyi kazi ya utakasaji. Hivyo ni nusu tu ya kazi ya Mungu ndiyo ilikuwa inafanywa, na kukamilisha kazi ya ukombozi ilikuwa ni nusu ya mpango Wake mzima. Kwa kuwa enzi mpya ilikuwa inakaribia kuanza na ile ya zamani kukaribia kutoweka, Mungu Baba Alianza kukusudia sehemu ya pili ya kazi Yake na Akaanza kujiandaa kwa ajili yake. Wakati uliopita, kupata mwili huku katika siku za mwisho huenda hakukutolewa unabii, na hivyo kuweka msingi wa usiri mkubwa unaozunguka ujio wa Mungu katika mwili kipindi hiki. Wakati wa mapambazuko, bila kujulikana kwa mtu yeyote, Mungu Alikuwa duniani na Akaanza maisha Yake katika mwili. Watu hawakujua kipindi hiki. Pengine wote walikuwa wamelala, pengine wengi waliokuwa wanakesha walikuwa wanasubiri, na pengine wengi walikuwa wanamwomba Mungu wa mbinguni kimyakimya. Lakini miongoni mwa watu hawa wote, hakuna hata mmoja aliyejua kuwa Mungu tayari Amekwishawasili duniani. Mungu Alifanya hivi ili Aifanye kazi Yake kwa urahisi na kupata matokeo bora zaidi, na pia ilikuwa ni kwa sababu ya kuepuka majaribu zaidi. Mwanadamu anapoamka kutoka usingizini, kazi ya Mungu itakuwa imekwishakamilika zamani sana na Ataondoka, na kufunga maisha Yake ya kutembeatembea na kusafiri duniani. Kwa kuwa kazi ya Mungu inamtaka Mungu kutenda na kuzungumza kwa nafsi Yake mwenyewe, na kwa kuwa hakuna namna ambayo mwanadamu anaweza kuingilia kati, Mungu Ameyavumilia maumivu makali ya kuja duniani kufanya kazi Yeye Mwenyewe. Mwanadamu hawezi kushikilia nafasi ya kazi ya Mungu. Kwa hiyo Mungu Alijihatarisha mara

elfu kadhaa kuliko ilivyokuwa katika wakati wa Enzi ya Neema na kuja chini mahali ambapo joka kuu jekundu linaishi ili kufanya kazi Yake, kuweka mawazo Yake yote na uangalizi katika kuokoa kundi hili la watu maskini, kulikomboa kundi hili la watu lililogeuka na kuwa rundo la samadi. Ingawa hakuna anayejua uwepo wa Mungu, Mungu Hahangaiki kwa sababu ni faida kubwa kwa kazi ya Mungu. Kila mtu ni mwovu sana, sasa inawezekanaje kila mtu avumilie uwepo wa Mungu? Ndiyo maana duniani, Mungu Anakuwa kimya siku zote. Haijalishi mwanadamu ni katili kiasi gani, Mungu wala Hazingatii hayo moyoni Mwake hata kidogo, bali Anaendelea kufanya kazi Anayotaka kufanya ili kutimiza agizo kuu ambalo Baba wa mbinguni Alimpatia. Ni nani miongoni mweni aliyetambua upendo wa Mungu? Ni nani anayejali sana mzigo Alionao Mungu Baba kuliko Mwana Wake Anavyofanya? Ni nani awezaye kuelewa mapenzi ya Mungu Baba? Roho wa Mungu Baba Aliyeko mbinguni Anasumbuka kila mara, na Mwana Wake duniani Anaomba mara kwa mara juu ya mapenzi ya Mungu Baba, Akihofia moyo Wake kuumia. Kuna mtu yeyote anayejua kuhusu upendo wa Mungu Baba kwa Mwana Wake? Kuna mtu yeyote anayejua jinsi ambavyo Mwana mpendwa Anavyomkumbuka Mungu Baba? Wakipata shida ya kuchagua kati ya mbingu na nchi, utaona wawili Hawa wanatazamana wakati wote kutoka kwa mbali, sambamba na Roho. Ee binadamu! Ni lini mtaufikiria moyo wa Mungu? Ni lini mtielewa nia ya Mungu? Baba na Mwana siku zote Wamekuwa Wakitegemeana. Kwa nini tena Watengane, mmoja juu mbinguni na mmoja chini duniani? Baba Anampenda Mwana Wake kama vile Mwana Anavyompenda Baba Yake. Kwa nini sasa asubiri kwa muda mrefu huku Akiwa na shauku hiyo? Ingawa Hawajatengana kwa muda mrefu, je, mtu yeyote anajua kwamba Baba tayari Amekuwa Akitaka sana kwa shauku kwa siku nyingi na Amekuwa Akitarajia kwa muda mrefu kurudi haraka kwa Mwana Wake mpendwa? Anatazama, Anakaa kwa utulivu, Anasubiri. Hii yote ni kwa ajili ya kutaka Mwana Wake mpendwa Arudi haraka. Ni lini Atakuwa tena na Mwana ambaye Anazungukazunguka duniani? Ingawa watakapokuwa pamoja tena, Watakuwa pamoja milele, Anawezaje kustahimili maelfu ya siku za utangano, mmoja juu mbinguni na mwingine chini duniani. Makumi ya miaka duniani ni kama maelfu ya miaka mbinguni. Mungu Baba Anawezaje kutokuwa na wasiwasi? Mungu Anapokuja duniani, Anakabiliana na mabadiliko mengi ya ulimwengu wa kibinadamu kama mwanadamu. Mungu Mwenyewe hana hatia, sasa kwa nini Mungu Ateseke kwa maumivu kama mwanadamu? Pengine ndiyo maana Mungu Baba Anatamani sana Mwana Wake Arudi haraka; nani awezaye kuujua moyo wa Mungu? Mungu Anampatia mwanadamu vitu vingi sana; mwanadamu anawezaje kuulipa moyo wa Mungu kikamilifu? Lakini mwanadamu anampatia Mungu kidogo sana; sasa Mungu Atawezaje kutokuwa na wasiwasi?

Ni wachache sana miongoni mwa wanadamu wanaouielewa moyo wa Mungu kwa sababu tabia za watu ni duni sana na hisia zao za kiroho zimepoa sana, na kwa sababu hawaoni wala kutilia

maanani kile ambacho Mungu anafanya. Hivyo Mungu Anaendelea kuwa na hofu juu ya mwanadamu, kana kwamba asili ya tabia ya wanyama ndani ya mwanadamu inaweza kuonekana muda wowote. Hii inaonyesha zaidi kwamba kuja kwa Mungu duniani kunaambatana na majaribu makubwa. Lakini kwa ajili ya kukamilisha kundi la watu, Mungu, Akiwa na utukufu, Alimwambia mwanadamu juu ya kila kusudi lake, bila kuficha kitu. Ameamua kwa dhati kukamilisha kundi hili la watu. Kwa hiyo, ije shida yoyote au jaribu, Anatazama mbali na kuyapuuzia yote. Anafanya kazi yake kimyakimya tu, Akiamini kwamba siku moja ambapo Mungu Atapata utukufu, mwanadamu atamjua Mungu, na kuamini kwamba mwanadamu atakapokuwa amekamilishwa na Mungu, atakuwa ameuelewa moyo wa Mungu kikamilifu. Sasa hivi kunaweza kuwepo watu wanaomjaribu Mungu au kumwelewa vibaya Mungu au kumlaumu Mungu; Mungu wala hayazingatii haya moyoni. Mungu atakapoingia katika utukufu, watu wote wataelewa kwamba kila kitu ambacho Mungu Anafanya ni kwa ajili ya mema ya binadamu, na watu wote wataelewa kwamba kila kitu ambacho Mungu Anafanya ni kwa sababu binadamu aweze kuishi vizuri. Ujio wa Mungu umeambatana na majaribu, na Mungu pia Anakuja katika adhama na ghadhabu Yangu. Muda ambapo Mungu Anamwacha mwanadamu, Atakuwa tayari Amapata utukufu, na Ataondoka Akiwa Amejawa na utukufu mwingi na furaha ya kurudi. Mungu Anayefanya kazi duniani Hazingatii mambo moyoni Mwake haijalishi watu wamemkataa kiasi gani. Yeye Anafanya tu kazi Yake. Uumbaji wa Mungu wa ulimwengu unaanzia mbali maelfu ya miaka huko nyuma, Amekuja duniani kufanya kazi isiyoweza kupimika, na Amapitia uzoefu mkubwa wa kukataliwa na kashfa. Hakuna anayekaribisha ujio wa Mungu; kila mtu anamwangalia tu kwa jicho kavu. Katika kipindi hiki cha maelfu ya miaka ya taabu, matendo ya mwanadamu yamevunjavunja moyo wa Mungu tangu zamani sana. Wala Hazingatii tena uasi wa watu, lakini badala yake Anatengeneza mpango tofauti ili kumbadilisha na kumsafisha mwanadamu. Dhihaka na kashfa, mateso, dhiki, mateso ya msalaba, kutengwa na wanadamu, na kadhalika ambayo Mungu Alipitia Akiwa katika mwili, Mungu Amapitia ya kutosha. Dhihaka na kashfa, mateso, dhiki, mateso ya msalaba, kutengwa na wanadamu, na kadhalika ambayo Mungu Alipitia Akiwa katika mwili, Mungu Amapitia ya kutosha. Mungu katika mwili Ameteseka kikamilifu na shida za ulimwengu wa wanadamu. Roho wa Mungu Baba wa mbinguni Aliona mambo hayo hayavumiliki na Akarudisha kichwa Chake nyuma na kufumba macho Yake, Akisubiri Mwana Wake mpendwa kurudi. Yote Anayoyatamani ni kwamba watu wote wasikie na kutii, waweze kuhisi aibu kubwa mbele ya mwili Wake, na wasiasi dhidi Yake. Anachokitamani ni kwamba watu wote waamini kwamba Mungu yupo. Aliacha zamani sana kutaka mambo makubwa kutoka kwa mwanadamu kwa sababu Mungu Amelipa gharama kubwa sana, lakini mwanadamu bado anajistarehesha,^[5] na kamwe haiweki kabisa kazi ya Mungu moyoni mwake hata kidogo.

Ingawa vitu Ninavyozungumzia leo juu ya kazi ya Mungu vinaweza kuwa na mengi ambayo ni ya upuuzi kimsingi,”^[6] hata hivyo kina makubwa yaliyo muhimu kwa kuingia kwa binadamu. Ninazungumza tu kiasi juu ya kazi na kisha kuzungumza kiasi juu ya kuingia, lakini kati ya vipengele hivi viwili, hakuna kisicho cha muhimu, na vikiunganishwa, vipengele hivi viwili ni vyenye manufaa zaidi kwa maisha ya mwanadamu. Hivi vipengele viwili ni vya kusaidiana^[7] na ni vyenye manufaa sana, vikiwezesha watu kuyaelewa bora mapenzi ya Mungu na kuwezesha mawasiliano kati ya watu na Mungu. Kupitia kwa majadiliano ya leo juu ya kazi, uhusiano wa watu na Mungu unaboresha zaidi, kuelewa kwa pande mbili kunaongezeka, na mwanadamu anaweza kuzingatia zaidi na kujali kwa mzigo wa Mungu; mwanadamu anaweza kuhisi kile ambacho Mungu anahisi, kuwa na ujasiri zaidi juu ya kubadilishwa na Mungu, na kusubiri kuonekana tena kwa Mungu. Hili ni ombi pekee la Mungu kwa mwanadamu leo—kuishi kwa kudhihirisha mfano wa mtu anayempenda Mungu, kuufanya ili kwamba mwanga wa kudhihirika kwa hekima ya Mungu utamulika katika enzi ya giza na ili kuishi kwa kudhihirisha kwa mwanadamu kuweze kuachaukurasa wa kung’aa katika kazi ya Mungu, uangaze milele katika Mashariki ya ulimwengu, ukiamuru uangalifu wa ulimwengu na uvutiwaji wa wote. Huku, kwa hakika, ni kuingia bora kwa wale wanaompenda Mungu leo.

Tanbihi:

1. “Wanapiga misuli na kujitayarisha kwa vita” imetumika kwa dhahaka.
2. “Isiyo ya kawaida” inamaanisha kwamba kuingia kwa watu kumeacha maadili na uzoefu wao unaegemea upande mmoja.
3. “Mwisho kabisa” kunamaanisha kwamba njia ambayo watu wanaifuata inaenda kinyume na mapenzi ya Mungu.
4. “Kubadilika kutokana na mtazamo wao wa kawaida” inahusu jinsi fikira za watu na maoni kumhusu Mungu hubadilika mara tu wanapokuja kumjua Mungu.
5. “Anajistarehesha” inamaanisha kwamba watu hawapendezwi kuhusu kazi ya Mungu na hawaizingatii kama muhimu.
6. “Upuuzi usio na msingi” linamaanisha kwamba kimsingi watu hawawezi kuafikia chanzo cha maneno anayosema Mungu na hawajui kile Anachokizungumzia. Msemo huu hutumiwa kwa kejeli.
7. “Kupeana mkono” kunamaanisha kwamba kuchanganya “kazi” na “kuingia katika ushirika” kutakuwa kwa manufaa zaidi kwa ujuzi wetu kumhusu Mungu.

Kazi na Kuingia (5)

Leo wote mnajua kwamba Mungu anawaongoza watu katika njia sahihi ya uzima, kwamba Anamwongoza mwanadamu kuchukua hatua inayofuata kuingia katika enzi nyingine, kwamba Anamwongoza mwanadamu kuvuka mipaka ya enzi hii ya kale ya giza, kutoka katika mwili, kutoka kwenye ukandamizaji wa nguvu za giza na ushawishi wa Shetani, ili kila mtu aweze kuishi katika ulimwengu wa uhuru. Kwa ajili ya kesho ya kupendeza, ili kwamba watu wawe

wakakamavu katika hatua zao kesho, Roho wa Mungu anapanga kila kitu kwa ajili ya mwanadamu, na ili mwanadamu aweze kuwa na furaha kubwa zaidi, Mungu anajitolea jitihada Zake zote katika mwili Akiandaa njia mbele ya mwanadamu, ili siku ambayo mwanadamu anaitamani sana iweze kuja haraka. Nyote mngeweza kufurahia wakati huu mzuri; si tendo rahisi kufanya mkutano na Mungu. Ingawa hamjawahi kumjua, tayari mmekuwa pamoja naye tangu kitambo. Laiti kila mtu angeweza kukumbuka milele siku zote hizi nzuri lakini fupi, na kuzifanya kuwa mambo yao ya kuwafurahisha duniani. Kazi ya Mungu tangu zamani imefichuliwa kwa mwanadamu—lakini kwa sababu mioyo ya watu ni yenye utata sana, na kwa sababu hawajawahi kuwa na shauku kwayo, kazi ya Mungu imebaki ikiwa imesitishwa juu ya msingi wake wa asili. Mawazo yao, fikira, na mtazamo wa akili, ingeonekana, inasalia iliyopitwa na wakati, kiasi kwamba mtazamo wa akili wa wengi wao unafanana na ule wa washenzi wa nyakati za kale, na haujabadilishwa hata kidogo. Kutokana na hilo, watu bado wamekanganyikiwa na hawajui kuhusu kazi ambayo Mungu anafanya. Wao hata hawajui zaidi kuhusu kile wanachofanya na kile wanachopaswa kuingia ndani. Mambo haya yanaleta matatizo makubwa kwa kazi ya Mungu na kuzuia maisha ya watu kwenda mbele. Kwa sababu ya kiini cha mwanadamu na ubora wake duni wa tabia, hawezi kuifahamu kazi ya Mungu, na kamwe hayachukulii mambo haya kuwa muhimu. Ikiwa mnataka maendeleo katika maisha yenu, lazima mwanze kuzingatia utondoti wa kuishi kwenu, mkifahamu kila mojawapo ili kudhibiti kuingia kwenu katika maisha, mbadilishe kabisa moyo wa kila mmoja wenu, na kutatua matatizo ya utupu ndani ya mioyo yenu na kuwepo kwa uchachu na kuchosha ambako kunawaumiza, ili kila mmoja wenu atafanywa upya kutoka ndani hadi nje na kufurahia kweli maisha ambayo yamerefushwa, ya miujiza, na huru. Lengo ni kwamba kila mmoja wenu ataweza kuwa hai, kuhuisha katika roho zenu, na kuwa na mfano wa kiumbe hai. Kati ya ndugu wote mnaowasiliana nao, ni mara chache kuna yeyote ambaye ni mwenye kuisimua na wa kupendeza. Wote ni kama sokwe watu wa kale, punguani na wajinga, inavyoonekana bila matarajio yoyote ya maendeleo. Jambo baya hata zaidi, ndugu ambao Nimewasiliana nao wamekuwa fidhuli na wasiostaarabika kama nduli wa mlimani. Hawajui chochote kuhusu tabia, seuze mambo ya msingi ya jinsi ya kutenda. Kuna dada wadogo wengi ambao, ingawa wanaweza kuonekana wenye akili na wenye sura nzuri, na wamekua wazuri kama maua, bado wanajiingiza katika mtindo “mbadala.” Nywele za dada^[a] mmoja zinaufunika uso wake wote, bila kuonyesha macho yake hata kidogo. Ingawa sehemu za uso wake ni safi na zenye heshima, mtindo wa nywele zake ni wa kukirihi, ukitoa hisi ya kuogofya, kama kwamba yeye ni mkosaji mkuu katika jela ya vijana. Macho yake, yaliyo meupe na maangavu kama zumaridi katika maji, yanasawazishwa na mavazi na mtindo wa nywele zake, na kuyafanya kuwa kama taa mbili, zinazoonekana ghafla usiku wa giza kuu, yanayomulika kwa vipindi kwa mng’aro wa kupofusha ambao hutia hofu katika mioyo ya wanaume, na bado inaonekana kana kwamba anajificha kwa

makusudi kutoka kwa mtu fulani. Wakati Ninapokutana naye, daima yeye hujaribu kupanga njia za kuondoka katika “mandhari” hayo, kama mwuaji ambaye amemwua mtu fulani na, kwa hofu kuu ya kupatikana, daima anakwepa; kwa hiyo, pia, yeye ni kama Waafrika weusi^[1] ambao wamekuwa watumwa kwa vizazi vingi na hawawezi kuinua vichwa vyao mbele ya wengine. Mpangilio huu maalum wa tabia, hadi jinsi watu hawa huvaa na kujinadhifisha, ingechukua miezi kadhaa ya kazi ili kuiboresha.

Kwa maelfu ya miaka, Wachina wameishi maisha ya utumwa na hii imebana sana fikira, mawazo, maisha, lugha, tabia, na matendo yao kiasi kwamba wamebaki bila uhuru wowote. Maelfu kadhaa ya miaka ya historia imewachukua watu muhimu waliomilikiwa na roho na kuwadhoofisha hadi kuwa kitu kinachofanana na maiti iliyoondokewa na roho. Wengi ni wale wanaoishi chini ya kisu cha kuchinja cha Shetani, wengi wanaishi katika makazi yanayofanana na pango la mnyama, wengi wanakula chakula kama wanachokula ng’ombe au farasi, wengi wapo katika mchafuko huko “ahera” na hawana maana kabisa. Katika umbo la nje, watu hawana tofauti na watu wa zamani, sehemu yao ya kupumzika ni kama kuzimu, na wote wanaowazunguka ni mashetani na pepo wachafu. Kwa umbo la nje, wanadamu wanaonekana kuwa ni “wanyama” wa tabaka ya juu; kwa kweli wanaishi na kukaa na mashetani wachafu. Bila mtu yeyote kuwashughulikia, watu wanaishi katika mtego uliojificha wa Shetani, na wamenaswa kabisa katika kazi zake za taabu kiasi kwamba hawawezi kutoroka. Hawakusanyiki na wapendwa wao katika makazi yao ya furaha, kuishi kwa furaha na kuyaishi maisha ya kuridhisha, bali wanaishi Kuzimu, wakishughulika na pepo na kushirikiana na mashetani. Kwa kweli, watu bado wamefungwa na Shetani, wanaishi mahali ambapo pepo wachafu wanakusanyika, na wanatawaliwa na hawa pepo wachafu, na ni kana kwamba vitanda vyao ni mahali ambapo maiti zao zimelala, kana kwamba ni sehemu zao za kustarehe. Uingiapo nyumbani kwao, uwanja ni baridi na pweke, upepo wa kuzizima ukipiga mluzi kupitia matawi makavu. Kufungua mlango kuelekea “eneo la kuishi,” chumba ni cheusi kabisa—ungeweza kunyoosha mkono wako na usione vidole vyako. Mwangaza mdogo unapenya ndani kupitia ufa katika mlango, ambao unafanya chumba kusononesha hata na kutisha hata zaidi. Mara kwa mara, panya hutoa vilio vyembamba vya ajabu, kana kwamba wanajifurahisha. Yote ndani ya chumba ni ya kutia kinyaa na ya kutisha, kama nyumba ambayo mtu aliyekuwa akiishi ndani amewekwa kwenye jeneza sasa hivi. Kitanda, mafarishi, na kabati dogo lisilo la kawaida ndani ya chumba vyote vimefunikwa kwa vumbi, chini kuna vigoda kadhaa vidogo vikikenua meno yao na kutia tahabibu kucha zao, na utando wa buibui unaning’inia juu ya kuta. Kioo kiko juu ya meza, kitana cha mbao kikiwa karibu nacho. Unapotembea kuelekea kwa kioo, unachukua mshumaa na kuuwasha. Unaona kwamba kioo kimefunikwa na vumbi, na kufanya aina ya “vipodozi” juu ya picha za watu^[2] ili kwamba wanaonekana kana kwamba wametoka kaburini hivi sasa. Kitana

kimejaa nywele. Vitu hivi vyote ni vya zamani na, visivyostaarabika na vinaonekana kana kwamba vimetumika hivi sasa na mtu aliyekufa hivi sasa. Ukiangalia kitana, unahisi kana kwamba kuna maiti iliyolala kwa upande mmoja. Nywele zilizo katika kitana, bila damu kuzunguka ndani yake, zina harufu ya wafu juu yake. Upepo wa kuzizima unaingia kupitia kwa ufa ulio katika mlango, kana kwamba pepo anajipenyeza kupitia kwa ufa, akirudi kuishi ndani ya chumba. Kuna mzizimo wa kukandamiza katika chumba, na ghafla, uvundo kama wa maiti inayooza, na kwa wakati huu inaweza kuonekana kuwa kuna mchanganyiko wa vitu vinavyoning'inia juu ya kuta, juu ya kitanda kuna matandiko yasiyo nadhifu, machafu na yenye harufu mbaya, kuna nafaka pembeni, kabati limefunikwa kwa vumbi, sakafu imefunikwa kwa matawi na uchafu, na kadhalika—kana kwamba vimetumika sasa hivi na mtu aliyekufa, akielemea mbele, akisaga meno yake na kupapura hewa. Hii inatosha kukutetemesha. Hakuna dalili ya uhai mahali popote katika chumba, chote ni giza na chenye unyevu, kama Kuzimu na jahanamu zilizotajwa na Mungu. Hili ni kama tu kaburi la mwanadamu, likiwa na kabati ambalo halijapakwa rangi, vigoda, viunzi vya madirisha, na milango iliyovishwa nguo za kuomboleza na kuwatukuza wafu kwa kimya. Mwanadamu amekuwa akiishi katika ahera hii kwa miongo kadhaa, au karne kadhaa, au hata milenia kadhaa, akienda nje mapema na kurudi akiwa amechelewa. Anajitokeza kwa “kaburi” lake alfajiri, wakati majogoo wanapowika, na kuangalia juu angani na kutazama chini ardhini, na kuanza shughuli zao za siku. Wakati jua linapotua, yeye hukokota mwili wake uliochoka na kurudi “kaburini”; kufikia wakati anapojaza tumbo lake inakuwa ni magharibi. Kisha, baada ya kumaliza maandalizi yake ya kuondoka “kaburini” tena keshoye, yeye huizima taa, ambayo inaonekana kutoa miali ya mioto ya mmemetuko. Wakati huu, yote ambayo yanaweza kuonekana chini ya mbalamwezi ni matuta ya makaburi yaliyoenea kama viduta vidogo katika kila pembe. Kutoka ndani ya “makaburi” inatokea sauti ya mikoromo ya mara kwa mara, ikiinuka na kushuka. Watu wote wanalala fofofu, na pepo wachafu na vizuka pia wanaonekana wakipumzika kwa amani. Mara kwa mara, mtu anasikia kunguru wakilia kutoka mbali—sauti ya vilio hivi vya huzuni katika usiku mtulivu na ulio kimya kama huu inatosha kusababisha kuwa na wasiwasi mkuu na kukuogofya sana.... Ni nani anayejua ni miaka mingapi waliyoishi katika mazingira kama haya, wakifa na kuzaliwa upya, nani ajuaye ni muda gani wamebakia katika ulimwengu wa binadamu ambapo watu na vizuka huchanganyika, na zaidi, ni nani anayejua mara ngapi wameuaga ulimwengu! Katika jahanamu hii iliyo duniani wanadamu huishi maisha ya furaha, kana kwamba hawana lalamiko hata moja, kwani kwa muda mrefu wamezoea maisha Kuzimuni. Na kwa hiyo, watu huvutiwa sana na mahali hapa ambapo pepo wachafu hukaa, kana kwamba pepo wachafu ni marafiki wao na wenzi wao, kana kwamba ulimwengu wa mwanadamu ni kikosi cha majambazi^[2]—kwani kiini cha asili cha mwanadamu kwa muda mrefu kimetoweka bila mnong'ono, kimepotea kisionekekane tena. Kuonekana kwa watu kuna kitu fulani cha pepo mchafu; zaidi ya hayo, matendo yao yanaendeshwa na pepo

wachafu. Leo, wao hawaonekani tofauti na pepo wachafu, ni kana kwamba walizaliwa kutoka kwa pepo wachafu. Zaidi ya hayo, watu pia wanapenda sana, na kuwaunga mkono, mababu zao. Hakuna ajuaye kwamba tangu wakati huo mwanadamu amekandamizwa sana na Shetani mpaka amekuwa kama sokwe milimani. Macho yao mekundu yana mtazamo wa kusihi, na katika nuru iliyofifia iangazayo kutoka kwao ni dalili hafifu ya uovu wa chuki wa pepo mchafu. Nyuso zao zimefunikwa na kunyanzi, zimepasuka kama ganda la msonobari, midomo yao inachomoza nje, kana kwamba imeundwa na Shetani, masikio yao yamefunikwa na masizi ndani na nje, migongo yao imepindwa, miguu yao inang'ang'ana kuhimili miili yao, na mikono yao myembamba inacheza nyuma na mbele kwa mahadhi safi. Ni kana kwamba ni ngozi na mfupa tu, lakini tena wao ni wanene kama dubu wa mlimani. Ndani na nje, wamejipamba na kuvaa kama sokwe kutoka nyakati za zamani—ni kana kwamba, leo, hawa sokwe bado hawajageuka kuwa na^[3] umbo la mtu wa kisasa, hivyo ndivyo walivyo nyuma!

Mwanadamu anaishi bega kwa bega na wanyama, na wanatembea pamoja kwa amani, bila ugomvi au vita vya maneno. Mwanadamu ni mgumu kuridhika vile anavyowajali na anavyohusika na wanyama, na wanyama wapo kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa mwanadamu, hasa kwa manufaa ya mwanadamu, bila wao kunufaika na chochote na kwa kumtii mwanadamu kikamilifu. Kwa namna zote, uhusiano kati ya mwanadamu na mnyama ni wa karibu^[4] na wa kukubaliana^[5]—na pepo wachafu, inaweza kuonekana, ni muungano kamilifu wa mwanadamu na mnyama. Hivyo, mwanadamu na pepo wachafu walio duniani hata ni marafiki wema zaidi na wasiotengana: Mwanadamu anaonekana kufarakana na pepo wachafu, lakini kimsingi ameunganika nao; wakati huo, pepo wachafu hawamnyimi mwanadamu kitu chochote, na “wanatoa” vyote walivyonavyo kwao. Kila siku, watu wanachacharika katika “kasri la mfalme wa kuzimu,” wakichezacheza na “mfalme wa kuzimu” (babu yao) na kutawaliwa naye, ili kwamba, leo, watu wamepakwa masizi, na, baada ya kuishi muda mrefu sana Kuzimuni, wana muda mrefu toka waache kutamani kurudi katika “dunia ya walio hai.” Hivyo, mara tu wanapoiona nuru, na kutazama matakwa ya Mungu, na tabia ya Mungu, na kazi ya Yake, wanahisi dukuduku na wasiwasi; bado wakitamani sana kurudi kuzimu na kuishi na mizimu. Walimsahau Mungu zamani sana, na hivyo wamekuwa wakizungukazunguka katika makaburi. Ninapokutana na mtu, Najaribu kuzungumza naye, na wakati huu tu ndipo Nagundua kwamba mtu aliyesimama mbele Yangu si mwanadamu kabisa. Nywele zake ni chafu, uso wake ni mchafu, na kuna kitu kama mbwa-mwitu kuhusu tabasamu lake la kuonyesha jino. Kwa hiyo, pia, anaonekana kuwa na ukorofi wa pepo ambaye ametoka tu kaburini na kumwona mwanadamu wa dunia iliyo hai. Mtu huyu daima hujaribu kuunda midomo yake kuwa tabasamu; inaonekana kuwa yenye kudhuru kwa siri na mbaya. Anaponionyesha tabasamu, ni kama kwamba ana jambo la kusema lakini anaonekana hana maneno ya kueleza, na kwa hiyo anaweza

tu kusimama upande mmoja, akionekana kukosa ufahamu na mjinga. Kutoka nyuma, anaonekana kuwasilisha “sura ya nguvu ya watu wa Kichina wanaofanya kazi”; nyakati hizi anaonekana wa kuchukiza sana hata zaidi, ukikumbuka sura ya vizazi vya Yan Huang/Yan Wang wa zamani^[c] ambavyo watu huzungumzia. Ninapomwuliza, anainamisha kichwa chake akiwa kimya. Inamchukua muda mrefu kujibu, na amejizuia sana anapofanya hivyo. Yeye hawezi kutuliza mikono yake, na anavinyonya vidole vyake viwili kama paka. Sasa tu ndio Natambua kwamba mikono ya yule mtu inaonekana kama kwamba imekuwa ikipekua katika takataka sasa hivi, na makucha yenye umbo lisilo sawa yaliyogeuka rangi sana kiasi kwamba mtu hawezi kamwe kujua kwamba yalitakiwa kuwa meupe, makucha “membamba” ambayo yamezungukwa sana na uchafu. Hata la kuchukiza zaidi, pande za nyuma za mikono yake zinafanana na ngozi ya kuku ambaye amenyonyolewa hivi sasa. Mistari iliyo mikononi mwao karibu yote imejaa thamani ya damu na jasho la kazi za mwanadamu, ndani ya kila mstari kuna kitu ambacho kinafanana na uchafu, kinachoonekana kuwa kinatoa “harufu nzuri ya udongo,” bora zaidi kuwakilisha thamani na kustahili kusifiwa kwa roho ya mwanadamu ya kuteseka—ili roho hii ya kuteseka imetiwa hata ndani zaidi ya kila mstari ulio juu ya mikono ya mwanadamu. Kutoka utosini hadi kidoleni, hakuna nguo anayovaa mwanadamu inayofanana na ngozi ya mnyama iliyo na manyoya, lakini hawajui kwamba, hata wakiwa “waheshimiwa” sana, thamani yao kwa kweli ni ya chini kuliko ile ya manyoya ya mbweha—chini, hata, kuliko unyoya mmoja wa tausi, kwa kuwa kwa muda mrefu nguo zake zimemfanya kuwa mbaya sana kiasi cha kuonekana mbaya kuliko nguruwe na mbwa. Vazi lake dogo mno la juu linaning’inia nusu chini ya mgongo wake, na miguu ya suruali yake ndefu—kama matumbo ya kuku—inaonyesha kwa ukamilifu ubaya wake kwa nuru ya jua yenye kung’aa. Nguo hizo ni fupi na nyembamba, kana kwamba kwa ajili ya kuonyesha kwamba miguu yake imefunguliwa kwa muda mrefu: Ni miguu mikubwa, sio tena “inchi tatu ya yungiyungi za dhahabu za inchi tatu” za jamii ya zamani. Mavazi ya mtu huyu yamefanywa ya kimagharibi sana, lakini pia ni duni mno. Nikutanapo naye, yeye daima ni mwenye haya, uso wake ukibubujika kwa wekundu, na hawezi kuinua kichwa chake kabisa, kana kwamba amekanyagiwa chini na pepo wachafu, na hawezi kuwa na ujasiri wa kuwaangalia watu usoni tena. Vumbi hufunika uso wa mwanadamu. Vumbi hili, ambalo limeanguka kutoka angani, linaonekana kuanguka kwa njia isiyo ya haki juu ya uso wa mwanadamu, na kuufanya uonekane kama manyoya laini ya jurawa. Macho ya mwanadamu ni kama ya jurawa, pia: madogo na makavu, bila mng’aro wowote. Anapozungumza, kwa kawaida kunena kwake ni kwa kusitasita na kuepaepa, kunachukiza sana na kuwaudhi wengine. Hata hivyo wengi huwatukuza watu hao kama “wawakilishi wa taifa.” Je, huu sio utani? Mungu anataka kuwabadilisha watu, kuwanusuru, kuwaokoa kutoka kwa kaburi la kifo, ili waweze kuepukana na maisha wanayoishi Kuzimu na jahanamu.

Tanbihi:

1. “Waafrica weusi” inahusu watu weusi ambao walilaaniwa na Mungu, ambao wamekuwa watumwa kwa vizazi vingi.
2. “Kikosi cha majambazi” ni sitiari inayomaanisha kundi la waovu. Inahusu upotovu wa wanadamu, na jinsi hakuna watu watakatifu miongoni mwa wanadamu.
3. Sentensi hii inahusu “mageuzi” ya sokwe watu kuwa na umbo la watu wa kisasa. Lengo ni la tashtiti: Hakuna, kwa kweli, kitu kama nadharia ya sokwe wa kale kugeuka kuwa wanadamu wanaotembea wima.
4. “Wa karibu” inatumiwa kwa dhihaka.
5. “Wa kukubaliana” inatumiwa kwa mzaha.
 - a. Maandishi ya asili yanasoma “Yeye.”
 - b. Maandishi ya asili yanasoma “nyuso za watu.”
 - c. “Yan” na “Huang” ni majina ya watawala wawili wa mithiolojia ambao walikuwa miongoni mwa watoaji wa kwanza wa utamaduni wa China. “Yan Wang” ni jina la Kichina la “mfalme wa kuzimu.” “Yan Huang” na “Yan Wang” yanakaribia kuwa homofonia yanapotamkwa katika lugha ya Mandarin.

Kazi na Kuingia (6)

Kazi na kuingia kwa uhalisia ni vya kiutendaji na vinarejelea kazi ya Mungu na kuingia kwa mwanadamu. Mwanadamu kukosa kabisa uelewa juu ya sura halisi ya Mungu na kazi ya Mungu kumesababisha shida kubwa katika kuingia kwake. Leo hii, watu wengi bado hawajui kazi ambayo Mungu anatimiza katika siku za mwisho, au kwa nini Mungu Anastahimili fedheha kubwa kupita kiasi kuja katika mwili na kusimama na mwanadamu katika makovu na majonzi. Mwanadamu hajui chochote kuhusu lengo la kazi ya Mungu, wala kusudi la mpango wa Mungu kwa ajili ya siku za mwisho. Kwa sababu mbalimbali, watu daima wanakuwa vuguvugu katika kuingia ambako Mungu anataka na wanabakia wenye shaka^[1], kitu ambacho kimeleta shida kubwa katika kazi ya Mungu katika mwili. Watu wanaonekana kuwa vizuizi na, leo hii, bado wanakuwa hawana uelewa sahihi. Kwa hiyo Nitazungumza juu ya kazi ambayo Mungu anafanya kwa mwanadamu, na makusudi ya Mungu ya haraka, ili kwamba nyinyi nyote muwe watumishi waaminifu wa Mungu ambao, kama Ayubu, ni bora ufe kuliko kumkataa Mungu na utastahimili kila fedheha, na ambao, kama Petro, mtatoa utu wenu wote kwa Mungu na kuwa wandani ambao Mungu Aliwapata katika siku za mwisho. Ninawasihi kaka na dada kufanya kila kitu kilichopo ndani ya uwezo wao kutoa utu wao wote kwa mapenzi ya mbingu ya Mungu, kuwa watumishi watakatifu katika nyumba ya Mungu, na kufurahia ahadi za kutokuwa na kikomo zilizotolewa na Mungu, ili kwamba moyo wa Mungu Baba ufurahie pumziko la amani. “Kukamilisha mapenzi ya Mungu Baba” kunapaswa kuwe wito wa wote wanaompenda Mungu. Maneno haya yanapaswa kutumika kama mwongozo wa mwanadamu kwa ajili ya kuingia na dira inayoongoza matendo yake. Hili ndilo suluhisho ambalo mwanadamu anapaswa kuwa nalo. Kukamilisha

kabisa kazi ya Mungu duniani na kushirikiana na kazi ya Mungu katika mwili—huu ni wajibu wa mwanadamu. Siku moja, kazi ya Mungu itakapokuwa imekamilika, mwanadamu atamuaga Anaporudi mapema kwa Baba yake mbinguni. Je, huu sio wajibu ambao mwanadamu anapaswa kuutimiza?

Wakati ambapo, katika Enzi ya Neema, Mungu alirudi kwa mbingu ya tatu, kazi ya Mungu ya kuwakomboa wanadamu wote ilikuwa kwa kweli tayari imeendelea katika tendo lake la kumaliza. Vyote vilivyobaki duniani vilikuwa msalaba ambao Yesu aliubeba, sanda ya kitani ambayo Yesu alifungiwa ndani, na taji ya miiba na joho la rangi nyekundu ambavyo Yesu alivaa (hivi vilikuwa vitu ambavyo Wayahudi walitumia kumdhihaki Yeye). Yaani, baada ya kazi ya kusulubiwa kwa Yesu isababishe mhemko mkubwa, mambo yalitulia tena. Tangu wakati huo na kuendelea, wanafunzi wa Yesu wakaanza kuendeleza kazi Yake, wakiyachunga na kunyunyizia katika makanisa kila mahali. Maudhui ya kazi yao yalikuwa haya: kuwafanya watu wote watubu, waungame dhambi zao, na wabatizwe; mitume wote wakienneza hadithi ya ndani ya kusulubiwa kwa Yesu na kile kilifanyika kwa kweli, kila mtu asiweze kujizua kuanguka chini mbele za Yesu kuungama dhambi zake, na zaidi ya hayo mitume wakienneza kila mahali maneno yaliyonenwa na Yesu na sheria na amri Alizozianzisha. Kuanzia wakati huo ujenzi wa makanisa ulianza katika Enzi ya Neema. Kile ambacho Yesu alizungumzia wakati wa enzi hiyo pia kililenga maisha ya mwanadamu na mapenzi ya Baba wa mbinguni. Ni kwa sababu tu enzi hizo ni tofauti ndiyo nyingi za semi na matendo hayo yanatofautiana sana na ya leo. Lakini kiini cha vyote viwili ni sawa. Yote mawili kwa uhakika na usahihi ni takriban kazi ya Roho wa Mungu katika mwili kabisa. Aina hii ya kazi na matamko yameendelea wakati wote mpaka siku hii, na kwa hivyo kitu cha aina hii bado kinashirikiwa kati ya mashirika ya dini leo na hakijabadilika hata kidogo. Wakati ambapo kazi ya Yesu ilikamilishwa, na makanisa tayari yalikuwa yameingia kwenye njia sahihi ya Yesu Kristo, Mungu bado alianzisha mpango Wake wa hatua nyingine ya kazi Yake, jambo la kupata mwili katika siku za mwisho. Kwa mwanadamu, Mungu kusulubiwa kulihitimisha kazi ya Mungu kupata mwili, Aliwakomboa binadamu wote, na Akamruhusu kuteka ufunguo wa Kuzimu. Kila mtu anadhani kwamba kazi ya Mungu imekamilika kikamilifu. Kwa uhalisia, kwa Mungu, ni sehemu ndogo tu ya kazi Yake ndiyo imekamilika. Amekomboa tu binadamu; Hajamshinda mwanadamu, wala kubadilisha ubaya wa Shetani kwa binadamu. Hiyo ndiyo maana Mungu Anasema, “Ingawa mwili Wangu ulipitia maumivu ya kifo, hilo sio lengo lote la Mimi kupata mwili. Yesu ni Mwana Wangu mpendwa na Alisulubishwa msalabani kwa ajili Yangu, lakini hakukamilisha kikamilifu kazi Yangu. Alifanya tu sehemu.” Hivyo Mungu Akaanza mpango wa mzunguko wa pili ili kuendeleza kazi ya Mungu kupata mwili. Lengo kuu la Mungu ni kumkamilisha na kumpata kila mmoja aokolewe kutoka katika mikono ya Shetani, hiyo ndiyo sababu Mungu Alijiandaa tena kujihatarisha kuja katika mwili. Maana ya

“kupata mwili” ni Yule ambaye haleti utukufu (kwa sababu kazi ya Mungu bado haijamalizika), lakini yule anayeonekana katika utambulisho wa Mwana mpendwa, na Yeye ndiye Kristo, ambaye Mungu amependezwa naye. Ndiyo maana hili linasemekana kuwa “kujitayarisha kwa ajili ya hatari”. Mwili ni wenye nguvu kidogo sana na lazima utahadhari sana,^[2] na nguvu Yake ni tofauti sana na mamlaka ya Baba wa mbinguni; Yeye hutimiza tu huduma ya mwili, Akifanikisha kazi na agizo la Mungu Baba bila kujihusisha katika kazi nyingine. Yeye hufanikisha tu sehemu moja ya kazi. Hii ndiyo maana Mungu anaitwa “Kristo” alipokuja duniani. Hii ndiyo maana ya ndani. Sababu ya kusema kwamba kuja huko kunaandamana na majaribu ni kwa kuwa mradi wa kazi mmoja pekee ndio unafanikishwa. Zaidi ya hayo, sababu Mungu Baba humwita tu “Kristo” na “Mwana mpendwa” na Hajampa utukufu wote ni hasa kwa vile mwili uliokuwa mwili huja kufanya mradi wa kazi moja, sio kumwakilisha Baba aliye mbinguni, bali kutimiza huduma ya Mwana mpendwa. Mwana mpendwa atakapomaliza agizo lote Alilokubali kubeba juu ya mabega Yake, Baba atampa Yeye utukufu kamili pamoja na utambulisho wa Baba. Mtu anaweza kusema kwamba hii ni kanuni ya mbinguni. Kwa sababu Yule ambaye amekuja katika mwili na Baba aliye mbinguni wako katika hali mbili tofauti, hao wawili huonana tu katika Roho, Baba akimtaazama kwa makini Mwana mpendwa lakini Mwana asiweze kumwona Baba kutoka mbali. Ni kwa sababu kazi ya mwili ni ndogo sana na Ana uwezo wa kuuawa wakati wowote, kwamba kuja huku kunasemekana kuambatana na hatari kuu. Hii ni sawa na Mungu mara tena kumwachilia Mwana Wake mpendwa na kumweka ndani ya mdomo wa chui mkubwa mwenye milia. Ni hatari kwa maisha kwamba Mungu alimweka Yeye mahali ambapo Shetani amekolea sana. Hata kwa kupata mashaka kama hayo, Mungu bado alimkabidhi Mwana Wake mpendwa kwa watu wa mahali pachafu, fisadi ili wao “wamlee.” Hii ni kwa sababu ni njia pekee ya kazi ya Mungu kuleta maana kabisa na njia pekee ya kutimiza mapenzi yote ya Mungu Baba na kufanikisha sehemu ya mwisho ya kazi Yake miongoni mwa wanadamu. Yesu alifanikisha tu hatua moja ya kazi ya Mungu Baba. Kwa sababu ya kizuizi cha mwili uliopata mwili na tofauti katika kazi iliyofanikishwa, Yesu Mwenyewe hakujua kwamba kungekuwa na kurudi kwa pili kwa mwili. Kwa hivyo hakuna mfafanuaaji au nabii wa Biblia aliyethubutu kutabiri wazi kwamba Mungu angepata mwili katika siku za mwisho, yaani, angekuja katika mwili tena ili kufanya sehemu ya pili ya kazi Yake katika mwili. Kwa hivyo, hakuna aliyetambua kwamba Mungu tayari Alikuwa amejificha kwa muda mrefu katika mwili. Si ajabu, kwani ilikuwa tu baada ya Yesu kufufuka na kupaa mbinguni ndipo Akakubali agizo hili, kwa hiyo hakuna unabii ulio wazi kuhusu kupata mwili kwa Mungu mara pili, na ni jambo lisilofikirika na akili ya binadamu. Katika vitabu vyote vingi vya unabii ndani ya Biblia, hakuna maneno yanayotaja hili kwa dhahiri. Lakini Yesu alipokuja kufanya kazi, tayari kulikuwa na unabii wa wazi uliosema kwamba bikira atashika uja uzito, naye atamzaa mwana, kumaanisha kwamba mimba Yake ilipatikana kwa njia ya Roho Mtakatifu. Hata hivyo, Mungu bado alisema

hili lilifanyika kwa hatari ya kifo, hivyo hali ingekuwaje ya hatari katika hali ya leo? Si ajabu Mungu asema kwamba kupata mwili wakati huu kuna hatari mara elfu zaidi kuliko zile za wakati wa Enzi ya Neema. Katika maeneo mengi, Mungu Alitabiri kupata kundi la washindi katika nchi ya Sinimu. Ni katika Mashariki mwa ulimwengu ambapo washindi watapatwa, hivyo nchi ambapo Mungu anashukia katika kupata mwili Kwake mara ya pili bila shaka ni nchi ya Sinimu, mahali ambapo joka jekundu linaishi. Hapo Mungu Atawapata warithi wa joka kuu jekundu na litashindwa na kuaibishwa. Mungu Anataka kuwaamsha watu hawa walioteseka sana, kuwaamsha kabisa, na kuwafanya waondoke katika ukungu na kulikataa joka kuu jekundu. Mungu Anataka Awaamshe kutoka katika ndoto zao, kuwafanya waelewe tabia ya joka kuu jekundu, kuutoa moyo wao wote kwa Mungu, kuinuka kutoka katika nguvu kandamizi za giza, kusimama Mashariki mwa dunia, na kuwa uthibitisho wa ushindi wa Mungu. Baada ya hapo Mungu Atakuwa Amapata utukufu. Kwa sababu hii tu, kazi ambayo ilisitishwa Israeli Mungu Aliipeleka katika nchi ambapo linakaa joka kuu jekundu na, takribani miaka elfu mbili baada ya kuondoka, Amekuja tena katika mwili ili kuendeleza kazi ya Enzi ya Neema. Mwanadamu anashuhudia kwa macho yake, Mungu Akizindua kazi mpya katika mwili. Lakini kwa Mungu, Anaendeleza kazi ya Enzi ya Neema, kwa mwachano wa miaka elfu kadhaa, na badiliko tu la eneo la kufanyia kazi na mradi wa kazi. Ingawa taswira ya mwili ambayo Mungu Ameichukua katika kazi ya leo ni mtu mwingine tofauti na Yesu, Wanashiriki hulka na mzizi mmoja, na wanatoka katika chanzo kimoja. Pengine wana tofauti za umbo la nje, lakini kweli za ndani za kazi Zao zinafanana kabisa. Hata hivyo, enzi zenyewe, ni tofauti kama ilivyo usiku na mchana. Inawezekanaje kazi ya Mungu isibadilike? Au inawezekanaje kazi ziingiliane?

Yesu alichukua umbo la Myahudi, Alifuata mavazi ya Wayahudi, na Alikua akila chakula cha Kiyahudi. Hii ni hali yake ya kawaida ya kibinadamu. Lakini Mungu katika mwili wa leo Anachukua umbo la watu wa Asia na Anakua katika taifa la joka kuu jekundu. Hii haiingiliani na lengo la Mungu kupata mwili. Badala yake, vinakamilishana, na zaidi vinakamilisha maana ya kweli ya Mungu kupata mwili. Kwa sababu Mungu katika mwili Anarejelewa kuwa “Mwana wa Adamu” au “Kristo,” umbo la nje la Kristo wa leo haliwezi kuzungumziwa kwa maneno sawa na Yesu Kristo. Hata hivyo, mwili huu unaitwa “Mwana wa Adamu” na Yupo katika sura ya mwili. Kila hatua ya kazi ya Mungu inahusisha maana ya kina sana. Sababu ya Yesu kuzaliwa kwa njia ya Roho Mtakatifu ni kwa sababu Alipaswa kuwakomboa wenye dhambi. Alitakiwa Asiwe na dhambi. Isipokuwa tu mwishoni Alipolazimishwa kufanana na mwili wa dhambi na kuchukua dhambi za wenye dhambi ndivyo Aliweza kuwaokoa kutoka katika laana ya msalaba ambao Mungu Alitumia kuwaadibu watu. (Msalaba ni zana ya Mungu kwa ajili ya kuwalaani na kuwarudi watu; mitajo ya kulaani na kurudi mahususi inahusu kuwalaani na kuwarudi wenye dhambi.) Lengo lilikuwa ni kuwafanya wenye dhambi wote kutubu na kutumia msalaba

kuwafanya waungame dhambi zao. Yaani, kwa ajili ya kuwakomboa binadamu wote, Mungu Alijiweka Mwenyewe katika mwili uliozaliwa kwa njia ya Roho Mtakatifu na Akachukua dhambi za binadamu wote. Namna ya kawaida ya kuelezea hii ni kutoa mwili mtakatifu kwa kubadilishana na wenye dhambi wote, usawa wa Yesu kuwa sadaka ya dhambi umewekwa mbele ya Shetani ili “kumsihi” Shetani kuwarudisha binadamu wote wasio na hatia kwa Mungu. Hivyo ili kukamilisha hatua hii ya kazi ya wokovu kulihitaji utungaji mimba kwa njia ya Roho Mtakatifu. Hili lilikuwa ni sharti la lazima, “mkataba” wakati wa vita kati ya Mungu Baba na Shetani. Hii ndio maana Yesu Alitolewa kwa Shetani, ni baada ya hapo tu ndipo hatua hii ya kazi ikahitimishwa. Hata hivyo, kazi ya ukombozi ya Mungu leo tayari ni ya umuhimu usio kifani, na Shetani hana sababu ya kufanya madai, hivyo Mungu kufanyika mwili hakuhitaji utungaji mimba kwa njia ya Roho Mtakatifu, maana Mungu kwa asili ni mtakatifu na Asiye na hatia. Hivyo Mungu mwenye mwili wa wakati huu sio tena Yesu wa Enzi ya Neema. Lakini bado Yupo kwa ajili ya mapenzi ya Mungu Baba na kwa ajili ya kutimiza matamanio ya Mungu Baba. Hii inaweza kuchukuliwaje kuwa ni msembo usiokuwa na maana? Je, ni lazima Mungu kupata mwili kufuate kanuni kadhaa?

Watu wengi wanatafuta ushahidi katika Biblia, wakitaka kutafuta unabii wa Mungu kupata mwili. Mwanadamu, na mawazo yake yaliyochanganyikiwa na kuvurugika, anawezaje kujua kwamba Mungu Aliacha “kufanya kazi” kwenye Biblia kitambo na “Ameruka” nje ya mipaka yake ili kwa bidii na hamu, Afanye kazi ambayo Alipanga kitambo lakini Hakuwahi kumwambia mwanadamu kuhusu? Watu wanakosa sana ufahamu. Baada tu ya kuonja tabia ya Mungu, kwa kawaida wanasimama kwenye jukwaa refu na kukaa kwenye “kiti mwendo” cha hali ya juu wakikagua kazi ya Mungu, na kwenda mbali zaidi kumfundisha Mungu kwa mazungumzo ya misamiati migumu. “Mzee” akiwa amevaa miwani na kupapasa ndevu zake, anafunua Biblia yake kuukuu ambayo amekuwa akiisoma maisha yake yote. Akimumunya maneno na kupepesapepesa macho, sasa anarudi katika Kitabu cha Ufunuo na sasa katika kitabu cha Danieli, na sasa katika Kitabu cha Isaya ambacho kinajulikana sana na kila mtu. Akikodolea macho ukurasa mmoja baada ya mwingine ulioandikwa maneno mengi madogo, anasoma kimya, akili yake ikizunguka bila kupumzika. Ghafula mkono unaopapasa ndevu unasita na kuanza kuzivuta. Kila mara mtu anasikia sauti ya ndevu zikivunjika. Tabia hiyo isiyo ya kawaida inamstaajabisha mtu. “Kwa nini kutumia nguvu zote hizo? Kilichomkasirisha hivyo ni nini?” Turudi kwa mtu mzee, nyusi zake sasa zimesimama. Nyusi zenye rangi ya fedha zimeanguka kama manyoya ya bata bukini sentimita mbili kamili kutoka katika kope za mzee huyu, kama tu kwa bahati lakini kwa usahihi kabisa, mzee huyu anaendelea kukaza macho yake kwenye kurasa zinazoonekana kana kwamba zimekumbwa na ukungu. Baada ya kurudia rudia kurasa zizo hizo mara kadhaa, hana budi ila kusimama upesi na kuanza kuropoka kana kwamba anafanya porojo^[3]

na mtu, ingawa mwanga unaotoka machoni mwake bado haujatoka katika shajara yake. Ghafula anafunika ukurasa aliokuwa anausoma na kugeukia “ulimwengu mwingine.” Mwendo wake ni wa haraka^[4] sana na wa kuogopesha takribani kuwashtua watu. Sasa, panya aliyekuwa ametoka katika shimo lake, wakati wa kimya chake, alikuwa anaanza tu kuhisi mtulivu kiasi cha kutembea kwa uhuru, anakuwa na wahaka sana kwa sababu ya mizunguko yake isiyotarajiwa kwamba anakimbia kwa wepesi kurudi kwenye shimo lake na kutoweka bila kujua alipoelekea. Sasa mkono wa kulia wa mzee uliokuwa umetulia unarudia mwendo wake wa kupapasa ndevu juu chini. Anaondoka kwenye kiti, na kuacha kitabu mezani. Kupitia katika mlango ulio wazi kidogo na dirisha lililo wazi, upepo unaingia ndani, bila kujali unapeperusha kitabu kinajifunika, kisha kinafunguka, kinajifunika, kisha kinafunguka tena. Kuna ukiwa usioweza kuelezeka kuhusu tukio hili, isipokuwa tu kwa sauti ya kurasa za kitabu zinapopeperushwa na upepo, kila kitu kinaonekana kuwa kimya. Yeye, pamoja na mikono aliyojikumbatia kwa nyuma, anatembeatembea chumbani, sasa anasimama, sasa anaanza, anatikisa kichwa chake mara kwa mara, anaonekana kurudia kusema “Ee! Mungu! Unaweza kweli kufanya hivyo?” Muda hadi muda pia anatikisa kichwa, “Ee Mungu! Nani anaweza kuijua kazi Yako? Ni vigumu kiasi gani kuchunguza hatua Zako? Ninaamini Hufanyi vitu visivyokuwa na maana.” Sasa mzee huyu anakunja uso, macho yake anayafumba kwa nguvu, akionyesha sura iliyokasirika, pia anaonyesha maumivu makali kupita kiasi, kana kwamba anataka kutafakari taratibu. Hii kweli inampatia changamoto “mzee huyu.” Katika hatua hii ya maisha yake, “kwa bahati mbaya” amekutana na suala hili. Nini kinaweza kufanyika juu yake? Nami pia sina nguvu ya kufanya kitu chochote. Nani alifanya shajara yake kuwa “ya njano”? Nani alifanya ndevu na nyusi zake kukua bila huruma kama theluji nyeupe katika maeneo mbalimbali ya uso wake? Ni kana kwamba ndevu zake zinawakilisha usuli wake. Lakini nani angejua mwanadamu angekuwa mpumbavu kwa kiasi hiki, akitafuta uwepo wa Mungu katika shajara kuukuu? Shajara hii ya zamani inaweza kuwa na karatasi ngapi? Je, inaweza kweli kurekodi matendo yote ya Mungu? Nani anathubutu kuhakikisha hilo? Ilhali mwanadamu kwa kweli anafikiria kutafuta kuonekana kwa Mungu na kutimiza mapenzi ya Mungu kwa njia ya kuchanganua maneno^[5] na kubishana juu ya tofauti ndogo ndogo, akitumai basi kuingia katika uzia. Je, kujaribu kuingia katika uzima kwa namna hii, ni rahisi kama inavyosikika? Je, huku sio kufikiri bila mantiki na kimakosa? Huoni hii inachekesha?

Tanbihi:

1. “Wenye shaka” inaashiria kwamba watu hawana umaizi dhahiri katika kazi ya Mungu.
2. “Ni wenye nguvu kidogo sana na lazima utahadhari sana” inaashiria kwamba ugumu wa mwili ni mwingi sana, na kazi iliyofanywa ni ndogo sana.
3. “Porojo” ni istiaara ya sura mbaya ya watu wanapochunguza katika kazi ya Mungu.

4. “Haraka” inamaanisha mwendo wa hamu na wa hima wa “mzee” anapoongelea kuhusu Biblia.

5. “Kuchanganua maneno” kunatumiwa kudhihaki wataalam katika hoja za uwongo, ambao hubishana juu ya tofauti ndogondogo kuhusu maneno lakini hawautafuti ukweli au kujua kazi ya Roho Mtakatifu.

Kazi na Kuingia (7)

Imemchukua mwanadamu mpaka siku hii kutambua kwamba kile mtu anachokosa si tu kuruzukiwa maisha ya kiroho na uzoefu wa kumjua Mungu, lakini, muhimu zaidi, mabadiliko katika tabia yake. Kutokana na ujinga kamili wa mwanadamu wa historia na utamaduni wa kale wa wanadamu, hana ujuzi wa kazi ya Mungu hata kidogo. Mwanadamu hutumaini kuwa ndani kabisa ya moyo, mwanadamu anaweza kumpenda Mungu kwa kina moyoni mwake, lakini kwa kuwa mwili wa mwanadamu umepotoshwa kwa kina sana, kwa kufa ganzi pamoja na kuwa usiohisi, hii imemsababisha kutojua chochote hata kidogo kumhusu Mungu. Mungu Anakuja miongoni mwa wanadamu siku ya leo kwa kusudi la kubadilisha mawazo na roho zao, na taswira ya Mungu katika mioyo yao ambayo wamekuwa nayo kwa mamilioni ya miaka. Kupitia fursa hii, Atamfanya mwanadamu kuwa mkamilifu. Yaani, kupitia maarifa ya mwanadamu, Atabadilisha namna wanavyomfahamu na mitazamo yao Kwake, ili kwamba maarifa yao juu ya Mungu, yaweze kuanza katika rekodi safi, na mioyo yao itakuwa imesafishwa upya na kubadilishwa. Kushughulika na nidhamu ni njia, na ushindi na kufanya upya ni malengo. Kuondoa mawazo ya kishirikina aliyonayo mwanadamu kuhusu Mungu asiye dhahiri ndilo limekuwa kusudi la Mungu milele, na hivi karibuni limekuwa suala la haraka kwake. Ingekuwa kwamba watu wote wangetafakari kwa kina kwa kuzingatia hali hii. Wabadilishe jinsi kila mtu anavyopitia uzoefu ili kwamba kusudi hili la haraka la Mungu liweze kufanyika hivi karibuni na hatua ya mwisho ya kazi ya Mungu duniani iweze kuhitimishwa kwa matokeo mazuri. Onyesheni uaminifu wenu kama mnavyopaswa, na ufariji moyo wa Mungu kwa mara ya mwisho. Ni matumaini Yangu kwamba hakuna mtu yeyote miongoni mwa kaka na dada atakayekwepa jukumu hili au kuzungukazunguka tu. Mungu Anakuja katika mwili wakati huu kwa mwaliko, na kutokana na hali ya mwanadamu. Yaani, Anakuja kumpatia mwanadamu kile alichokuwa anahitaji. Atakuja kumwezesha kila mwanadamu, wa tabia yoyote au jamii, kuona neno la Mungu na, kutoka katika neno Lake, kuona uwepo na udhihirishaji wa Mungu na kukubali ukamilishaji wa Mungu. Neno lake litabadilisha mawazo na mitazamo ya mwanadamu ili kwamba sura ya kweli ya Mungu ikite mizizi kabisa katika moyo wa mwanadamu. Hili ndilo tamanio pekee la Mungu duniani. Haijalishi jinsi gani asili ya mwanadamu ilivyo, jinsi gani asili yake ilivyo duni, au matendo yake yalivyokuwa huko nyuma, Mungu Hajali haya. Anatumainia tu mwanadamu kuisafisha kabisa taswira ya Mungu aliyonayo moyoni mwake na kuijua asili ya binadamu, na hapo Atakuwa Amebadilisha mtazamo wa kiitikadi wa mwanadamu. Anatarajia mwanadamu kuwa na shauku ya kina kwa Mungu na kuwa na mahusiano ya milele na Yeye.

Hiki ndicho Mungu Anachomwomba mwanadamu.

Maarifa ya utamaduni wa kale na historia ambayo imekuwepo kwa maelfu kadhaa ya miaka imefunga fikra na mawazo na akili yake mwanadamu kwa nguvu sana kiasi cha kuzifanya kutowezakana kupenyezwa na kutoweza kuoza.^[1] Watu wanaishi katika duara la kumi na nane la kuzimu, kana kwamba wamefukuziwa chini na Mungu, wasiweze kuona mwanga tena. Fikra za kishirikina hivyo zimewakandamiza watu kiasi kwamba hawawezi kupumua na wana shida ya kupumua. Hawana nguvu hata kidogo ya kupinga, kimya kimya wanaendelea kuvumilia na kuvumilia... Hakuna hata mmoja aliyewahi kujaribu kupigana au kusimama kwa ajili ya uadilifu na haki; watu wanaishi maisha ambayo ni mabaya zaidi ya mnyama, chini ya kugongwa na unyanyasaji wa maadili ya kishirikina, siku baada ya siku na mwaka baada ya mwaka.

Wanadamu hajawahi kufikiria kumtafuta huyu Mungu ili kufurahia furaha katika ulimwengu wa mwanadamu. Ni kana kwamba mwanadamu amepigwa, kama majani yaliyoanguka ya majira ya kupukutika, yaliyonyauka na kukauka kabisa. Mwanadamu amepoteza kumbukumbu na anaishi bila matumaini kuzimu kwa jina la ulimwengu wa kibinadamu, akisubiri ujio wa siku ya mwisho ili kwamba waweze kupotea pamoja na kuzimu, kana kwamba siku ya mwisho wanayoitamani sana ni siku watakayofurahia pumziko la amani. Maadili ya kishirikina yamempeleka mwanadamu “Kuzimu,” hivyo kudhoofisha zaidi uwezo wa mwanadamu wa kupinga.

Ukandamizaji wa aina mbalimbali umemlazimisha mwanadamu taratibu kuzama chini kabisa Kuzimu na kutanga mbali kabisa na Mungu. Sasa, Mungu Amekuwa mgeni kabisa kwa mwanadamu, na mwanadamu bado anafanya haraka kumwepuka wanapokutana. Mwanadamu hamtilii maanani na anamtenga kana kwamba mwanadamu hajawahi kumwona hapo kabla. Bado Mungu amekuwa mwenye subira kwa mwanadamu wakati wote katika safari ndefu ya maisha ya binadamu, kamwe harushi ghadhabu Yake isiyoweza kusitishwa kwake, Amekuwa Akisubiri tu kimya tu, bila kunena lolote, kwa mwanadamu kutubu na kuanza upya. Mungu zamani alikuja kwenye ulimwengu wa binadamu na Huvumilia mateso hayo hayo kama mwanadamu. Ameishi na mwanadamu kwa miaka mingi na hakuna aliyegundua kuwepo Kwake. Mungu huvumilia tu kwa kimya taabu ya uchakavu katika ulimwengu wa binadamu huku Akifanya kazi Aliyoleta yeye mwenyewe. Anaendelea kuvumilia kwa ajili ya mapenzi ya Mungu Baba na kwa ajili ya mahitaji ya wanadamu, Amevumilia, Akipitia maumivu ambayo kamwe mwanadamu hajawahi kupitia. Mbele ya mwanadamu, Amewahudumia kimya kimya na kujinyenyekeza Mwenyewe, kwa ajili ya mapenzi ya Mungu Baba na mahitaji ya wanadamu. Maarifa ya utamaduni wa kale kwa taratibu yamemwondoa mwanadamu kutoka katika uwepo wa Mungu na kumweka mwanadamu kwa mfalme wa mashetani na wana wake. Vitabu Vinne na Maandiko Matano Bora^[a] vimepeleka fikira za mwanadamu na mawazo yake katika enzi nyingine ya uasi, na kumfanya mwanadamu kuendelea kuwaabudu wale walioandika Vitabu hivyo na Maandiko ya

Kiyunani, wakikuza zaidi mitazamo yao juu ya Mungu. Kwa ukosefu wa kujua wa mwanadamu, mfalme wa mashetani bila huruma alimtupa Mungu nje ya moyo wake na kuumiliki yeye mwenyewe kwa furaha ya ushindi tangu wakati huo, mwanadamu akawa na roho mbaya na ya uovu akiwa na uso wa mfalme wa mashetani. Chuki juu ya Mungu ilijaza kifua chao na sumu ya mfalme wa mashetani ikasambaa ndani ya mwanadamu hadi alipomalizwa kabisa. Mwanadamu hakuwa tena hata na chembe ya uhuru na hakuwa na njia ya kujikwamua kutokana na taabu za mfalme wa mashetani. Hakuwa na budi ila kuchukuliwa mateka papo hapo, kujisalimisha na kuanguka chini kwa kutii mbele yake. Hapo zamani, wakati moyo na nafsi ya mwanadamu vilikuwa vichanga, mfalme wa mashetani alipanda ndani yake mbegu ya saratani ya ukanaji Mungu ndani ya moyo mchanga wa mwanadamu, akimfundisha mwanadamu dhana za uongo kama vile, “kujifunza sayansi na teknolojia, kutambua Vipengele Vinne vya Usasa, hakuna Mungu duniani.” Si hivyo tu, ametangaza kwa kurudiarudia, “Hebu tujenge makazi mazuri sana kwa kufanya kazi kwa bidii,” akiwaomba wote kujiandaa toka wakiwa watoto kutumikia nchi yao. Mwanadamu amepelekwa mbele yake bila kujitambua, na bila kusita akajichukulia sifa (akimrejelea Mungu akiwa Ameshikilia binadamu mzima katika mikono Yake). Hajawahi kuwa na kuhisi aibu yoyote au kuwa na hisia yoyote ya aibu. Aidha, bila aibu amewanyakua watu wa Mungu na kuwaweka katika nyumba yake, wakati akirukaruka kama panya mezani na kumfanya mwanadamu amwabudu kama Mungu. Ni ujahili kabisa huu Anaropoka tuhuma hizo za kushtua, “Hakuna Mungu duniani. Upepo upo kwa ajili ya sheria za asili; mvua ni unyevunyevu unaoganda na kudondoka chini kama matone; tetemeko la ardhi ni mtikisiko wa uso wa ardhi kwa sababu ya mabadiliko ya jiolojia; ukame ni kwa sababu ya ukavu hewani kwa mwingiliano wa kinyuklia katika uso wa jua. Haya ni matukio ya asili. Ni sehemu gani ambayo ni tendo la Mungu?” Kuna wale hata wanaofoka kauli kama zifuatazo, kauli ambazo hazifai kutamkwa. “Mwanadamu alitoka kwa nyani katika nyakati zilizopita, na dunia leo inatoka kwa mfululizo wa jamii zizizostaarabika kuanzia takribani miaka mingi isiyohesabika. Iwapo nchi inaendelea au inaanguka inaamuliwa na mikono ya watu wake.” Kwa nyuma, inamfanya mwanadamu kuning’iniza kwenye ukuta au kuweka kwa meza ili kutoa heshima na kumtolea sadaka. Wakati huo huo anapiga kelele kwamba “Hakuna Mungu,” anajichukulia mwenyewe kuwa ni Mungu, na kumsukumia mbali Mungu nje ya mipaka ya dunia bila huruma. Anasimama katika sehemu ya Mungu na kutenda kama mfalme wa mashetani. Ni upuuzi mkubwa kiasi gani! Anamsababisha mtu kuteketezwa na chuki yenye sumu. Inaonekana kwamba Mungu ni adui wake mkubwa na Mungu Hapatani naye kabisa. Anafanya hila zake za kumfukuza Mungu wakati anabakia huru na hajapatikana.^[2] Huyu kweli ni mfalme wa mashetani! Tunawezaje kuvumilia uwepo wake? Hatapumzika hadi awe ameisumbua kazi ya Mungu na kuiacha katika matambara na kuwa katika hali ya shaghalabaghala kabisa,^[3] kana kwamba anataka kumpinga Mungu hadi mwisho, hadi mmoja kati yao awe ameangamia. Anampinga Mungu kwa makusudi na kusogea karibu zaidi.

Sura yake ya kuchukiza imefunuliwa toka zamani na sasa imevilia damu na kugongwagongwa,^[4] ipo katika hali mbaya sana, lakini bado hapunguzi hasira zake kwa Mungu, kana kwamba anatamani kummeza Mungu kabisa kwa mara moja ili kutuliza hasira moyoni mwake. Tunawezaje kumvumilia, huyu adui wa Mungu anayechukiwa! Ni kumalizwa kwake na kuondolewa kabisa ndiko kutaleta kutimia kwa matamania yetu ya maisha. Anawezaje kuruhusiwa kuendelea kukimbia ovyoovyo? Amemharibu mwanadamu kwa kiwango kama hicho mwanadamu hajui 'mahali pa raha zote, na amekuja kuwa mfu na asiye na hisia. Mwanadamu amepoteza uwezo wa kawaida wa kufikiri wa kibinadamu. Kwa nini tusitoe nafsi zetu zote kumwangamiza yeye na kumchoma ili kuondoa kabisa hofu yote ya hatari ya siku zijazo na kuruhusu kazi ya Mungu kuufikia uzuri usiotarajiwa mapema? Genge hili la waovu limekuja katika dunia ya wanadamu na kusababisha hofu na shida kubwa. Wamewaleta wanadamu wote katika ukingo wa jabali, wakipanga kwa siri kuwasukumia chini wavunjike vipande vipande na kumeza maiti zao. Wana matumaini ya kuharibu mpango wa Mungu na kushindana na Mungu katika pambano ambalo ana nafasi ndogo sana ya kushinda.^[5] Hiyo kwa vyovyote vile ni rahisi! Msalaba umeandaliwa, mahususi kwa ajili ya mfalme wa mashetani ambaye ni mwenye hatia ya makosa maovu sana. Mungu si wa msalaba tena na Amekwishamwachia Shetani. Mungu Aliibuka mshindi muda mrefu uliopita, Hahisi tena huzuni juu ya dhambi za binadamu. Ataleta wokovu kwa binadamu wote.

Kutoka juu hadi chini na kutoka mwanzo hadi mwisho, Shetani amekuwa akivuruga kazi ya Mungu na kutenda katika upinzani Kwake. Mazungumzo yote ya “urithi wa utamaduni wa kale,” “maarifa ya thamani ya utamaduni wa kale,” “mafundisho ya imani ya Tao na imani ya Confucius,” na “maandiko ya kale ya Confucius na ibada ya kishirikina” vimempeleka mwanadamu kuzimu. Sayansi na teknolojia ya kisasa, vilevile maendeleo ya viwanda, kilimo, na biashara havionekeni popote. Badala yake, anasisitiza ibada za kishirikina zilizoenezwa na “masokwe” wa kale kwa makusudi kabisa kuingilia, kupinga na kuharibu kazi ya Mungu. Sio tu amemtesa mwanadamu hadi leo hii, bali anataka kummaliza^[6] mwanadamu kabisa. Mafundisho ya maadili ya kishirikina na kurithisha maarifa ya utamaduni wa kale vimemwambukiza mwanadamu kwa muda mrefu na kumbadilisha mwanadamu kuwa mashetani wakubwa na wadogo. Kuna wachache sana ambao wapo tayari kumpokea Mungu na kukaribisha kwa furaha ujio wa Mungu. Uso wa mwanadamu umejawa na mauaji, na katika sehemu zote, kifo kipo hewani. Wanatafuta kumwondoa Mungu katika nchi hii; wakiwa na visu na mapanga mikononi, wanajipanga katika pambano kumwangamiza Mungu. Sanamu zimetapakaa nchi nzima ya shetani ambapo mwanadamu anafundishwa kuwa hakuna Mungu. Juu ya nchi hii kunatoka harufu mbaya sana ya karatasi linaloungua na ubani, ni harufu nzito sana inayomaliza hewa. Inaonekana kuwa ni harufu ya uchafu unaopeperuka wakati joka anapojisogeza na kujizungusha,

na ni harufu ambayo mwanadamu hawezi kuvumilia bali kutapika tu. Licha ya hiyo, kunaweza kusikika pepo waovu wakikariri maandiko. Sauti inaonekana kutoka mbali kuzimu, na mwanadamu hawezi kujizua kusikia baridi ikiteremka chini ya uti wake. Katika nchi hii sanamu zimetapakaa, zikiwa na rangi zote za upinde wa mvua, ambazo zinaibadilisha nchi kuwa ulimwengu ya furaha ya kutamanisha, wakati mfalme wa mashetani ameendelea kucheka vibaya, kana kwamba njama zake za kupotosha zimefanikiwa. Wakati huo mwanadamu hana habari naye, wala mwanadamu hajui kwamba shetani amekwishamharibu kwa kiwango ambacho amekuwa hawezi kuhisi na ameshindwa. Anatamani, kwa kishindo, kuangamiza kila kitu kuhusu Mungu, na kwa mara nyingine kuchafua na kumwangamiza; nia yake ni kubomoa na kuvunja kazi Yake. Anawezaje kumruhusu Mungu kuwa wa hadhi sawa? Anawezaje kumvumilia Mungu “akiingilia” na kazi yake miongoni mwa wanadamu ulimwenguni? Anawezaje kumruhusu Mungu kuufichua uso wake wa kutisha? Anawezaje kumruhusu Mungu kuingilia kazi yake? Inawezekanaje Shetani huyu anayevimba kwa ghadhabu, amruhusu Mungu kuwa na utawala juu ya mahakama yake ya kifalme duniani? Anawezaje kukubali kushindwa kwa urahisi? Sura yake ya chuki imefunuliwa wazi, hivyo mtu anajikuta hajui kama acheke au alie, na ni vigumu sana kuzungumzia hili. Hii si asili yake? Akiwa na roho mbaya, bado anaamini kwamba yeye ni mzuri kupita kiasi. Genge hili la washiriki jinai!^[7] Wanakuja miongoni mwa walio na mwili wa kufa na kuendeleza starehe na kuvuruga mpangilio. Usumbufu wao unaleta kigeugeu duniani na kusababisha hofu katika moyo wa mwanadamu, na wamemchezea mwanadamu sana kiasi kwamba mwonekano wake umekuwa ule wa mnyama wa mashambani, mbaya sana, na kutoka athari ya mwisho ya mwanadamu asilia imepotea. Aidha, wanatamani kuwa wa nguvu za ukuu duniani. Wanakwamisha kazi ya Mungu kiasi kwamba isiweze kusonga mbele kiasi kidogo na wanamfunga mwanadamu kwa mkazo kama wapo nyuma ya kuta za shaba na chuma cha pua. Baada ya kufanya dhambi mbaya sana na kusababisha majanga mengi sana, je, bado wanatarajia kitu tofauti na kuadibu? Mapepo na roho wa Shetani wamekuwa wakicharuka duniani na wamefunga mapenzi na jitihada za maumivu za Mungu, na kuwafanya wasiweze kupenyeka. Ni dhambi ya mauti kiasi gani! Inawezekanaje Mungu Asiwe na wasiwasi? Inawezekanaje Mungu Asiwe na ghadhabu? Wanasababisha vikwazo vya kusikitisha na upinzani kwa kazi ya Mungu. Uasi wa kutisha! Hata mapepo hao wadogo kwa wakubwa wanajivunia nguvu za Shetani mwenye nguvu zaidi na kuanza kufanya fujo. Kwa makusudi wanapinga ukweli licha ya kuuelewa vizuri. Wana wa uasi! Ni kana kwamba, sasa mfalme wao amepanda kwenda katika kiti cha enzi cha kifalme, wamekuwa wa kuridhika nafsi na kuwatendea wengine wote kwa dharau. Ni wangapi wanautafuta ukweli na kufuata haki? Wote ni wanyama kama tu nguruwe na mbwa, wakuongoza genge la nzi wanaonuka katika rundo la kinyesi na kuchomeka vichwa vyao na kuchochea vurugu.^[8] Wanaamini kwamba mfalme wao wa kuzimu ni mkuu kuliko mfalme wa wote, kujua kidogo kwamba wao si zaidi ya nzi wenye uvundo. Na bado, wanatumia vibaya

uwezo wa nguruwe na mbwa ambao ni wazaziwe ili kukashifu uwepo wa Mungu. Kama nzi wadogo, wanaamini wazazi wao ni wakubwa kama nyangumi wenye meno.^[9] Hawatambui kwamba wao ni wadogo sana, ilihali wazazi wao ni nguruwe wachafu mara mamia ya mamilioni kuliko wao wenyewe kwa ukubwa? Hawatambui uduni wao, wanacharuka kwa misingi ya harufu iliyooza ya nguruwe na mbwa hao na wana mawazo ya udanganyifu ya kuzaa vizazi vijavyo. Huko ni kukosa aibu kabisa! Wakiwa na mbawa za kijani mgongoni mwao (hii inarejelea wao kudai kuwa wanamwamini Mungu), wanaanza kuwa na majivuno na kiburi juu ya uzuri wao na mvuto wao, kwa siri kabisa wanamtupia mwanadamu uchafu wao. Na hata ni wa kuridhika nafsi, kana kwamba jozi ya mbawa zenye rangi ya upinde wa mvua zingeweza kuficha uchafu wao, na kwa njia hizi wanaleta ukandamizaji kwa uwepo wa Mungu wa kweli (hii inarejelea yale yanayoendelea kwa nyuma katika ulimwengu wa kidini). Ni jinsi gani mwanadamu angejua kwamba, licha ya urembo mzuri wa mbawa za nzi, nzi mwenyewe ni kiumbe mdogo tu, aliye na tumbo iliyojaa uchafu na mwili uliojaa vijidudu? Kwa kutegemea uwezo wa nguruwe na mbwa wa wazazi wao, wanacharuka nchi nzima (hii inarejelea viongozi wa dini wanaomtesa Mungu kwa misingi ya uungwaji mkono mkubwa kutoka katika nchi inayomsaliti Mungu wa kweli na ukweli) kwa ukatili uliopitiliza. Ni kana kwamba mizimu ya Mafarisayo wa Kiyahudi wamerudi pamoja na Mungu katika nchi ya joka kuu jekundu, wamerudi katika kiota chao cha zamani. Wameanza tena mkondo mwingine wa usaliti, wakianzisha kazi yao yenye miaka maelfu kadhaa iliyopita. Kikundi hiki cha waliopotoka ni hakika kitaangamia duniani hatimaye! Inaonekana kwamba, baada ya milenia kadhaa, roho wachafu wamekuwa wenye hila na wadanganyifu sana. Muda wote wanafikiri juu ya njia za kuidhoofisha kazi ya Mungu kwa siri. Ni werevu sana na wajanja na wanatamani kurudia katika nchi yao kufanya majanga yaliyotokea maelfu kadhaa ya miaka iliyopita. Hii takribani imfanye Mungu kulia kwa sauti kuu, na Anajizuia sana kurudi katika mbingu ya tatu ili Awaangamize. Kwa mwanadamu kumpenda Mungu ni lazima aelewe mapenzi Yake na furaha Yake na huzuni, vilevile na kile Anachokichukia zaidi. Hii itakuza zaidi kuingia kwa mwanadamu. Kadiri mwanadamu anavyoingia kwa haraka, ndivyo moyo wa Mungu unavyoridhika zaidi; kadiri mwanadamu anavyomtambua kwa uwazi mfalme wa mashetani, ndivyo mwanadamu anavyosogea karibu zaidi na Mungu, ili kwamba matamano Yake yaweze kutimia.

Tanbihi:

1. “Kutoweza kuoza” imenuiwa kama tashtiti hapa, kumaanisha kwamba watu ni wagumu katika ufahamu, utamaduni na mitizamo yao ya kiroho.
2. “Huru na hajapatikana” inaonyesha kwamba shetani anapagawa na kucharuka.
3. “Hali ya shaghalabaghala kabisa” inahusu jinsi tabia ya shetani ya ukatili haivumiliki kuona.
4. “Imevilia damu na kugongwagongwa” inahusu sura mbaya ya kutisha ya mfalme wa pepo.

-
5. “Pambano ambalo ana nafasi ndogo sana ya kushinda” ni istara ya mipango mibaya ya shetani yenye kudhuru kwa siri, ya uovu. Inatumiwa kwa dhihaka.
 6. “Kummaliza” inahusu tabia ya kidhalimu ya mfalme wa pepo, ambaye huwaangamiza watu wote.
 7. “Washiriki jinai” ni wa namna moja na “kundi la majambazi.”
 8. “Kuchochea vurugu” inahusu jinsi watu ambao wana pepo husababisha ghasia, kuzuia na kuipinga kazi ya Mungu.
 9. “Nyangumi mwenye meno” imetumiwa kwa dhihaka. Ni istara ya jinsi nzi ni wadogo sana kiasi kwamba nguruwe na mbwa huonekana wakubwa kama nyangumi kwao.
- a. Vitabu Vinne na Maandiko Matano Boara ni vitabu vyenye mamlaka ya Ukonfushashi nchini China.

Kazi na Kuingia (8)

Nimezungumza mara nyingi sana kwamba kazi ya Mungu ya siku za mwisho ni kwa ajili ya kubadilisha roho ya kila mtu, kubadilisha nafsi ya kila mtu, ili kwamba moyo wake, ambao umeteseka sana na kiwewe, uwe umebadilishwa, hivyo kuokoa nafsi yake, ambayo imeumizwa kwa kina zaidi na uovu; ni kwa sababu ya kuamsha roho za watu, kuyeyusha mioyo yao baridi, na kuwaruhusu kurudisha nguvu za ujana. Haya ndiyo mapenzi makubwa ya Mungu. Weka pembeni mazungumzo ya ni namna gani maisha na uzoefu wa mwanadamu ni ya kiburi au ya kina; mioyo ya watu itakapokuwa imeamshwa, wanapokuwa wameamshwa kutoka kwa ndoto zao na kujua kikamilifu madhara yaliyoletwa na joka kuu jekundu, kazi ya huduma ya Mungu itakuwa imekamilika. Siku ambayo kazi ya Mungu itakuwa imekamilika pia ni siku ambapo mwanadamu atanza rasmi kwenye njia sahihi ya kumwamini Mungu. Wakati huu, huduma ya Mungu itakuwa imekamilika: Kazi ya Mungu katika mwili itakuwa imekamilika kabisa, na mwanadamu atakuwa ameanza rasmi kufanya kazi ambayo anapaswa kufanya—atatekeleza huduma yake. Hizi ni hatua za kazi ya Mungu. Hivyo mnapaswa kutafuta kwa kupapasa kuingia kwenu katika misingi ya kujua mambo haya. Haya yote ndiyo mnayopaswa kuyajua. Kuingia kwa mwanadamu kutaboreka tu pale ambapo mabadiliko yatatokea ndani kabisa ya moyo wake, maana kazi ya Mungu ni wokovu kamili wa mwanadamu—mwanadamu aliyekombolewa, ambaye bado anaishi chini ya nguvu za giza, na ambaye hajawahi kuzinduka kutoka katika eneo hili la kusanyiko la pepo; ili kwamba mwanadamu aweze kuwekwa huru dhidi ya milenia ya dhambi, na kuwa wapendwa wa Mungu, kumkanyaga kabisa joka kuu jekundu, kuanzisha ufalme wa Mungu, na kuupumzisha moyo wa Mungu mapema, ni kutoa mawazo bila woga, bila kubania, kwa chuki inayovimbisha kifua chenu, kuondoa kabisa vijidudu hivyo, kuwafanya muache maisha haya ambayo hayana tofauti na maisha ya ng’ombe au farasi, ili msiwe watumwa tena, ili msiweze kukanyagwa tena au kuamrisha na joka kuu jekundu; hamtakuwa tena wa taifa hili lililoanguka, hamtakuwa tena wa joka kuu jekundu lenye chuki, hamtafungwa nalo tena. Kiota cha pepo hakika kitachanwachanwa na Mungu, na mtasimama kando ya Mungu—nyinyi

ni wa Mungu, na sio wa milki hii ya watumwa. Mungu ameichukia sana jamii hii ya giza toka zamani. Anasaga meno Yake, Akitamani kumkanyaga mwovu huyu, joka wa zamani mwenye chuki, ili kwamba asiinuke tena, na hatamnyanyasa tena mwanadamu; Hatasamehe matendo yake ya zamani, Hatavumilia udanganyifu wake kwa mwanadamu, atalipiza kisasi kwa kila kosa alilofanya katika enzi zote. Mungu hatamsamehe hata kidogo huyu kiongozi wa uovu wote,^[1] Atamwangamiza kabisa.

Kwa maelfu ya miaka hii imekuwa ni nchi ya uchafu, ni chafu sana, shida zimejaa, mizimu wanakimbia kila mahali, wakihadaa na kudanganya, wakitoa tuhuma zisizokuwa na msingi,^[2] wakiwa katili na waovu, wakikandamiza mji huu ulio mahame na kuuacha ukiwa umetapakaa maiti; harufu ya uozo inaijaza nchi na kuenea hewani, na inalindwa isivyo kawaida.^[3] Nani awezaye kuuona ulimwengu kupita anga? Ibilisi anaufunga mwili wote wa mwanadamu, anafumba macho yake yote, na kufunga kinywa chake kwa nguvu. Mfalme wa pepo amefanya ghasia kwa maelfu kadhaa ya miaka, hadi leo hii, wakati bado anaangalia kwa karibu mji ulio mahame kana kwamba ulikuwa kasiri la pepo lisilopenyeka; kundi hili la walinzi, wakati uo huo, wakiangalia kwa macho yanayong'aa, wakiogopa sana kwamba Mungu atawakamata bila wao kujua na kuwafutilia wote mbali, Akiwaacha wakiwa hawana sehemu ya amani na furaha. Inawezekanaje watu wa mji wa mahame kama huu wawe wamewahi kumwona Mungu? Je, wamekwishawahi kufurahia uzuri na upendo wa Mungu? Wanathamini vipi masuala ya ulimwengu wa kibinadamu? Ni nani miongoni mwao anayeweza kuelewa matakwa ya kina ya Mungu? Haishangazi, basi, kwamba Mungu mwenye mwili abaki kuendelea kuwa Amefichwa: Katika jamii ya giza kama hii, ambapo pepo hawana huruma na ni katili, inawezekanaje mfalme wa pepo anayewa watu bila hisia yoyote, avumilie uwepo wa Mungu ambaye ni mwenye upendo, mpole, na mtakatifu? Anawezaje kushangilia na kufurahia ujio wa Mungu? Vikaragosi hawa! Wanalipa upole kwa chuki, wanamtweza Mungu kwa muda mrefu, wanamtukana Mungu, ni washenzi kupita kiasi, hawamjali Mungu hata kidogo, wanapora na kuteka nyara, wamepoteza dhamiri yote, wanaenda kinyume na dhamiri yote, na wanawajaribu watu wasiokuwa na hatia kuwa watu wasiokuwa na uwezo wa kuhisi. Wazazi wa kale? Viongozi Wapendwa? Wote wanampinga Mungu! Udukuzi wao umeacha wote walio chini ya mbingu katika hali ya giza na machafuko! Uhuru wa dini? Haki halali na matakwa ya wananchi? Zote hizo ni njama za kufunika dhambi! Nani ambaye ameikumbatia kazi ya Mungu? Nani ametoa maisha yake au kumwaga damu kwa ajili ya kazi ya Mungu? Kwa kizazi baada ya kizazi, kutoka kwa wazazi hadi watoto, mwanadamu aliyepo katika utumwa bila heshima amemfanya Mungu mtumwa—hii inawezaje kukosa kuamsha hasira? Maelfu ya miaka ya chuki ikiwa imejaa kifuani, milenia ya dhambi imeandikwa katika moyo—inawezekanaje hii isichochee chuki? Kumlipiza Mungu, kuuondoa kabisa uadui wake, usimwache kutangatanga tena, na usimruhusu kufanya fujo zaidi

kama anavyotaka! Sasa ndio wakati: Mwanadamu ana muda mrefu tangu akusanye nguvu zake zote, amejitolea nguvu zake zote, amelipa kila gharama, kwa hili, kuchana uso uliojificha wa pepo hili na kuwafanya watu, ambao wamepofushwa na kuvumilia kila aina ya mateso na taabu, kuinuka kutoka katika maumivu na kurudi kwa ibilisi huyu wa zamani. Kwa nini uweke kikwazo hicho kisichopenyeka katika kazi ya Mungu? Kwa nini utumie hila mbalimbali kuwadanganya watu wa Mungu? Uhuru wa kweli na haki na matakwa halali vipo wapi? Usawa uko wapi? Faraja iko wapi? Wema upo wapi? Kwa nini utumie mbinu za hila kuwadanganya watu wa Mungu? Kwa nini utumie nguvu kukandamiza ujio wa Mungu? Kwa nini usimruhusu Mungu kuzunguka katika dunia ambayo Ameiumba? Kwa nini umsumbue Mungu hadi Anakosa sehemu ya kupumzisha kichwa Chake? Wema upo wapi miongoni mwa wanadamu? Ukarimu upo wapi miongoni mwa wanadamu? Kwa nini usababishe matamano makubwa kiasi hicho kwa Mungu? Kwa nini umfanye Mungu kuita tena na tena? Kwa nini umlazimishe Mungu kuwa na wasiwasi kwa sababu ya Mwana Wake mpendwa? Katika jamii hii ya giza, kwa nini mbwa wao walinzi wasimruhusu Mungu kuja bila kizuizi na kuzunguka dunia ambayo Aliiumba? Kwa nini mwanadamu haelewi, mwanadamu anayeishi katika maumivu na mateso? Mungu amevumilia mateso makubwa kwa ajili yenu, kwa maumivu makubwa Amemtoa Mwanawe wa pekee, mwili wake na damu, kwa ajili yenu, sasa kwa nini bado mnakuwa vipofu? Katika mtazamo mzima wa kila mtu, mnakataa ujio wa Mungu, na mnakataa urafiki wa Mungu. Kwa nini mnakosa busara kiasi hicho? Mko tayari kuvumilia uonevu katika jamii ya giza kama hii? Kwa nini, badala ya kujaza tumbo lenu kwa milenia ya uadui, mnajidanganya wenyewe kwa “kinyesi” cha mfalme wa pepo?

Je, vikwazo kwa kazi ya Mungu ni vikubwa vipi? Je, kuna yeyote aliyewahi kujua? Watu wakiwa wamefungwa tunduni na rangi za ushirikina zenye nguvu, ni nani anayeweza kuujua uso wa kweli wa Mungu? Kwa ujuzi huu wa kitamaduni wenye maendeleo ya nyuma mno ulio wa juujuu na wa upuuzi, wangewezaje kuelewa kwa ukamilifu maneno yaliyosemwa na Mungu? Hata wakati wanapozungumziwa ana kwa ana, na kulishwa, mdomo kwa mdomo, wangewezaje kuelewa? Wakati mwingine ni kana kwamba maneno ya Mungu yamepuuzwa kabisa: Watu hawana mjibizo hata kidogo, wao hutikisa vichwa vyao na hawaelewi chochote. Je, hili lingekosaje kuwa lenye kutia wasiwasi? Hii “historia ya kitamaduni ya kale na maarifa ya kitamaduni ya mbali^[4]” imekuza kikundi cha watu wasio na thamani hasa. Utamaduni huu wa kale—urithi wa thamani—ni rundo la takataka! Uligeuka kuwa aibu ya milele kitambo, na haustahili kutajwa! Umewafundisha watu hila na mbinu za kumpinga Mungu, na “mwongozo wa utaratibu, wa upole”^[5] wa elimu ya kitaifa umewafanya watu kuwa wakaidi hata zaidi kwa Mungu. Kila sehemu ya kazi ya Mungu ni ngumu sana, na kila hatua ya kazi Yake duniani imekuwa ya kumhuzunisha Mungu. Jinsi kazi Yake duniani ilivyo ngumu! Hatua za kazi ya

Mungu duniani zinahusisha shida kubwa: Kwa ajili ya udhaifu wa mwanadamu, upungufu, utoto, ujinga na kila kitu cha mwanadamu, Mungu hufanya mipango yenye uangalifu na hufikiria kwa makini. Mwanadamu ni kama duma wa kutisha ambaye mtu hathubutu kumtega au kumchokoza; anapoguswa tu anauma, au vinginevyo anaanguka chini na kupoteza mwelekeo wake, na ni kana kwamba, akipoteza umakini kidogo tu, anarudia uovu tena, au anampuuza Mungu, au anakimbia kwa wazazi wake walio kama nguruwe na mbwa kuendeleza mambo machafu ya miili yao. Ni kizuizi kikubwa kiasi gani! Katika kila hatua ya kazi Yake, Mungu anakabiliwa na ushawishi, na takribani katika kila hatua Mungu anakumbana na hatari kubwa. Maneno yake ni ya kweli na ya uaminifu, na bila uovu, lakini nani yupo tayari kuyakubali? Nani yupo tayari kutii kikamilifu? Inavunja moyo wa Mungu. Anafanya kazi usiku na mchana kwa ajili ya mwanadamu, Anasongwa na wasiwasi kuhusu maisha ya mwanadamu na Anauonea huruma udhaifu wa mwanadamu. Amevumilia shida nyingi katika kila hatua ya kazi Yake, kwa kila neno Analozungumza; Yupo katikati ya mwamba na sehemu ngumu, na kufikiria juu ya udhaifu wa mwanadamu, ukaidi, utoto, na vile alivyo hatarini wakati wote ... tena na tena. Nani amewahi kulijua hili? Nani anaweza kuwa na imani? Nani anaweza kufahamu? Anachukia dhambi za wanadamu daima, na ukosefu wa uti wa mgongo, mwanadamu kutokuwa na uti wa mgongo, ndiko kunamfanya kuwa na hofu juu ya hatari aliyonayo mwanadamu, na kutafakari njia zilizopo mbele ya mwanadamu; siku zote, anapoangalia maneno na matendo ya mwanadamu, je, yanamjaza huruma, hasira, na siku zote vitu hivi vinamletea maumivu moyoni Mwake. Hata hivyo, wasio na hatia wamekuwa wenye ganzi; kwa nini ni lazima Mungu siku zote afanye vitu kuwa vigumu kwao? Mwanadamu dhaifu, ameondolewa kabisa uvumilivu; kwa nini Mungu awe na hasira isiyopungua kwa mwanadamu? Mwanadamu aliye dhaifu na asiye na nguvu hana tena uzima hata kidogo; kwa nini Mungu anamkaripia siku zote kwa ukaidi wake? Nani anayeweza kuhimili matishio ya Mungu mbinguni? Hata hivyo, mwanadamu ni dhaifu, na yupo katika dhiki sana, Mungu ameisukuma hasira Yake ndani kabisa moyoni Mwake, ili kwamba mwanadamu ajiakisi mwenyewe taratibu. Ilhali mwanadamu, aliyepo katika matatizo makubwa, hazingatii hata kidogo mapenzi ya Mungu; amedondoshwa miguuni na mfalme mzee wa pepo, na bado haelewi kabisa, siku zote anajiweka dhidi ya Mungu, au si moto wala baridi kwa Mungu. Mungu amezungumza maneno mengi sana, lakini nani ambaye ameyazingatia? Mwanadamu haelewi maneno ya Mungu, lakini bado hashtuki, bila kuwa na shauku, na hajawahi kuelewa kabisa hulka ya ibilisi wa kale. Watu wanaishi Kuzimu, lakini wanaamini wanaishi katika kasri la chini ya bahari; wanateswa na joka kuu jekundu, lakini bado wanadhani “wamependelewa”^[6] na nchi; wanadhihakiwa na ibilisi lakini wanadhani wanafurahia ustadi wa hali ya juu wa mwili. Ni wachafu kiasi gani, ni mafidhuli kiasi gani! Mwanadamu amekutana na bahati mbaya, lakini haijui, na katika jamii hii ya giza anapatwa na ajali baada ya ajali,^[7] lakini hajawahi kufahamu hili. Ni lini atakapoachana na wema wake wa kibinafsi na tabia ya mawazo ya kiutumwa? Kwa

nini hajali moyo wa Mungu kiasi hicho? Je, anajifanya haoni ukandamizaji na shida hii? Je, hatamani kuwe na siku ambayo atabadilisha giza kuwa nuru? Je, hatamani zaidi kuponya uonevu dhidi ya haki na ukweli? Je, yupo tayari kutazama tu bila kufanya chochote watu wakitupilia mbali ukweli na kupindua ukweli? Je, anafurahia kuendelea kuvumilia matendo haya mabaya? Je, yupo radhi kuwa mtumwa? Je, yupo tayari kuangamia mkononi mwa Mungu pamoja na watumwa wa taifa hili lililoanguka? Azma yako ipo wapi? Malengo yako yapo wapi? Heshima yako ipo wapi? Maadili yako yapo wapi? Uhuru wako upo wapi? Je, uko tayari kutoa maisha yako yote⁽⁸⁾ kwa ajili ya joka kuu jekundu, mfalme wa pepo? Je, unafurahi kumwacha akutese hadi kufa? Kina chake ni vurugu na giza, ilhali mtu wa kawaida, anayeteseka na mateso kama hayo, analalamika bila kupumzika. Ni lini mwanadamu ataweza kunyanyua kichwa chake juu? Mwanadamu amekuwa kimbaumbau na amekonda, anawezaje kuridhika na ibilisi huyu katili na dikteta? Kwa nini asiyatoe maisha yake kwa Mungu mapema awezavyo? Kwa nini bado anayumbayumba? Anaweza kumaliza kazi ya Mungu lini? Hivyo anaonewa na kunyanyaswa bila sababu yoyote, maisha yake yote hatimaye yatakuwa bure; kwa nini ana haraka hivyo ya kufika, na haraka hiyo ya kuondoka? Kwa nini hahifadhi kitu kizuri cha kumpa Mungu? Je, amesahau milenia ya chuki?

Labda, watu wengi huchukia sana baadhi ya maneno ya Mungu, au labda hawayachukii sana wala hawana shauku kwayo. Hata hivyo, ukweli hauwezi kugeuka kuwa kufikiri kwa upuuzi; hakuna anayeweza kusema maneno ambayo yanaupinga ukweli. Mungu amefanyika kuwa mwili wakati huu kufanya kazi hii, kukamilisha kazi ambayo bado Hajaikamilisha, kuifunga enzi hii, kuihukumu enzi hii, kuwaokoa waliozama kabisa dhambini kutoka katika ulimwengu wa bahari ya mateso na kuwabadilisha kabisa. Wayahudi walimsulubisha Mungu msalabani, hivyo kuhitimisha safari za Mungu kwenda Uyahudi. Sio baada ya muda mrefu, Mungu mwenyewe Alikuwa kwa wanadamu kwa mara nyingine tena, na kuwasili kimyakimya katika nchi ya joka kuu jekundu. Kimsingi, jumuiya ya kidini ya serikali ya Kiyahudi kwa muda mrefu ilikuwa imetundika picha ya Yesu katika kuta zao, na kwa vinywa vyao watu wakalia “Bwana Yesu Kristo.” Hawakujua kwamba Yesu alikubali zamani sana amri ya Baba Yake kurudi miongoni mwa wanadamu kukamilisha hatua ya pili ya kazi Yake ambayo haikuwa imekamili bado. Na matokeo yake, watu walipigwa na butwaa walipomwangalia: Alikuwa Amezaliwa katika ulimwengu ambamo enzi nyingi zilikuwa zimepita, na Alionekana miongoni mwa wanadamu kwa umbo la yule ambaye ni wa kawaida kabisa. Kimsingi, kadri enzi zilivyopita, mavazi Yake na umbo lote vimembadilika, kana kwamba Amezaliwa upya. Watu wangewezaje kujua kuwa ni Bwana Yesu Kristo yule Aliyeshuka msalabani na Aliyefufuliwa? Hana hata chembe ya jeraha, kama ambavyo Yesu hakuwa Anafanana na Yehova. Yesu wa leo kwa muda mrefu hajakuwa na kuvumilia kwa nyakati zilizopita. Watu wangewezaje kumjua? Watu wenye mashaka kama

“Tomaso” mnafiki siku zote anakuwa na mashaka kwamba ni Yesu aliyefufuka, na siku zote anataka kuona makovu ya misumari katika mikono ya Yesu kabla hajatuliza akili yake; bila kuyaona, siku zote anaweza kusimama katika wingu la mashaka, na anakuwa hana uwezo wa kusimama imara na kumfuata Yesu. Maskini “Tomaso”—angewezaje kujua kuwa Yesu amekuja kufanya kazi Aliyoamriwa na Mungu Baba? Kwa nini Yesu anataka kuchukua makovu ya msalaba? Je, makovu ya kusulubiwa ni alama za Yesu? Amekuja kufanya kazi kwa ajili ya mapenzi ya Baba Yake; kwa nini Aje Akiwa Amevaa na kupambika kama Myahudi wa miaka elfu kadhaa iliyopita? Je, umbo ambalo Mungu analichukua katika mwili linaweza kuzuia kazi ya Mungu? Je, hii ni nadharia ya nani? Kwa nini, Mungu anapofanya kazi, ni lazima iwe kulingana na mitazamo ya mwanadamu? Kitu cha pekee ambacho Mungu anazingatia ni katika kazi Yake ni ili kazi hiyo iwe na matokeo. Hafuati sheria, na hakuna kanuni katika kazi Yake—mwanadamu angewezaje kuielewa? Mwanadamu anawezaje kupenya kikamilifu kazi ya Mungu kwa kutegemea fikira na mawazo yake? Hivyo itakuwa heri kwenu kutulia vizuri: Msihangaike na mambo madogomadogo, na msichukulie kwa ukubwa mambo ambayo ni mapya kwenu—hii itakuzuia kujitania na watu kukucheka. Umemwamini Mungu kwa miaka yote hii lakini bado humjui Mungu; hatimaye unatumbukiza katika kuadibu, wewe, ambaye umewekwa katika “kiwango cha juu kabisa,”^[9] umewekwa katika madaraja ya walioadibiwa. Ni bora zaidi usitumie mbinu zako za kijanja kuonyesha hila zako; je, mtazamo wako huo finyu unaweza kumwelewa Mungu, Anayefahamu kutoka milele hadi milele? Je, uzoefu wako wa juujuu unaweza kukuruhusu ubaini kabisa mapenzi ya Mungu? Usiwe na majivuno. Hata hivyo, Mungu sio wa dunia—kwa hiyo inawezekanaje kazi Yake iwe kama ulivyotarajia?

Tanbihi:

1. “Kiongozi wa uovu wote” inahusu ibilisi mkongwe. Kirai hiki kinaonyesha kutopenda kabisa.
2. “Wakitoa tuhuma zisizokuwa na msingi” inahusu mbinu ambazo ibilisi hutumia huwadhuru watu.
3. “Inalindwa isivyo kawaida” inaonyesha kuwa mbinu ambazo ibilisi hutumia huwatesa watu ni mbovu hasa, na kuwadhibiti watu sana kiasi kwamba hawana nafasi ya kusogea.
4. “Ya mbali” inatumiwa kwa dhihaka.
5. “Mwongozo wa utaratibu, wa upole” imetumika kimzaha.
6. “Wamependelewa” inatumiwa kuwadhihaki watu wanaonekana wagumu na hawajitambui.
7. “Anapatwa na ajali baada ya ajali” inaonyesha kuwa watu walizaliwa katika nchi ya joka kubwa jekundu, na hawawezi kuwa na ujasiri.
8. “Kutoa maisha yako yote” imetumika kwa namna ya kimatusi.
9. “Kiwango cha juu kabisa,” inatumiwa kuwadhihaki wale wanaomtafuta Mungu kwa bidii.

Kazi na Kuingia (9)

Tamaduni za asili na mitazamo ya kiakili madhubuti vimeweka kivuli katika roho safi na ya kitoto ya mwanadamu, vimeshambulia roho ya mwanadamu bila ubinadamu hata kidogo kana kwamba anaondolewa hisia na hali yoyote ya nafsi. Mbinu za mashetani hawa ni za kikatili kupita kiasi, na ni kana kwamba “elimu” na “malezi” vimekuwa ni njia za kitamaduni ambazo kwazo mfalme wa mashetani anamchinja mwanadamu; kwa kutumia “mafundisho yake ya kina” anafunika kabisa roho yake mbaya, akivaa mavazi ya kondoo ili kupata imani ya mwanadamu na kisha kuchua fursa mwanadamu akilala fofofu kwa uchovu ili kummeza kabisa. Masikini binadamu—wangewezaje kujua kwamba nchi ambayo kwayo wamelelewa ni nchi ya Shetani, kwamba aliyewalea kimsingi ni adui ambaye anawaumiza. Lakini bado mwanadamu hazinduki kabisa; baada ya kushibisha hasira na kiu chake, anajiandaa kulipa “wema” wa wazazi wake kwa kumlea. Hivyo ndivyo mwanadamu alivyo. Leo, bado hajui kwamba “mfalme” ambaye alimlea ni adui yake. Nchi imechafuliwa na mifupa ya wafu, Shetani anafanya wazimu bila kutulia, na anaendelea kumeza mwili wa mwanadamu huko “kuzimu,” akishiriki kaburi pamoja na mifupa ya wanadamu na akijaribu waziwazi kuwamaliza masalia wa mwisho wa mwili wa mwanadamu uliobakia matambara. Lakini mwanadamu bado ni mjinga, na hajawahi kumchukulia Shetani kama adui yake, lakini badala yake anamtumikia kwa moyo wake wote. Watu kama hao waliokengeuka hawawezi kumjua Mungu. Ni rahisi kwa Mungu kuwa mwili na kuja miongoni mwa wanadamu, Akitekeleza kazi Zake zote za wokovu? Mwanadamu, ambaye tayari amekwishajiingiza Kuzimu, anawezaje kukidhi matakwa ya Mungu? Mungu amevumilia sana kulala bila kupata usingizi kwa ajili ya kazi ya binadamu. Kutoka vina vya juu hadi vya chini, Amepanda kwenda katika kuzimu ambapo mwanadamu anaishi kupitisha siku Zake na mwanadamu, hajawahi kulalamikia uchakavu walionao wanadamu, hajawahi kumlaumu kwa ukaidi wake, lakini Anavumilia mateso makuu kadri Anavyofanya kazi Yake. Inawezekanaje Mungu awe wa kuzimu? Inawezekanaje Aishi maisha Yake kuzimu? Lakini kwa ajili ya binadamu wote, ili binadamu wote waweze kupata pumziko mapema zaidi, Amestahimili fedheha na kupitia udhalimu kuja duniani, na Aliingia mwenyewe “jahanamu” na “kuzimu,” katika tundu la duma, kumwoko mwanadamu. Mwanadamu amestahili vipi kumpinga Mungu? Ana sababu gani tena ya kumlaumu Mungu? Anawezaje kuwa na ujasiri wa kumwangalia Mungu tena? Mungu wa mbinguni Amekuja katika nchi hii chafu zaidi ya uovu, na Hajawahi kutangaza manung’uniko au malalamiko Yake kuhusu mwanadamu, lakini badala yake Anakubali kimyakimya maangamizi^[1] na ukandamizaji wa mwanadamu. Kamwe Hajawahi kujibu matakwa ya mwanadamu yasiyokuwa na msingi, hajawahi kutaka mambo mengi yanayomuelemea mwanadamu, na hajawahi kumwekea mwanadamu matakwa yasiyokuwa na msingi; Anafanya tu kazi ambazo mwanadamu alitakiwa kufanya bila malalamiko: kufundisha,

kutia mwanga, kukaripia, usafishaji wa maneno, kukumbusha, kusihi, kufariji, kuhukumu na kufunua. Ni hatua gani Alizozichukua ambazo si kwa ajili ya maisha ya mwanadamu? Ingawa Ameondoa matarajio na majaliwa ya mwanadamu, ni hatua zipi zilizochukuliwa na Mungu ambazo hazikuwa kwa ajili ya majaliwa ya mwanadamu? Ni ipi kati ya hatua hizo ambayo haijawahi kuwa kwa ajili ya mwanadamu kuendelea kuishi? Ni ipi kati ya hatua hizo haijakuwepo kwa ajili ya kumweka mwanadamu huru dhidi ya mateso haya na kunyanyaswa na nguvu za giza ambazo ni nyeusi kama usiku? Ni ipi kati ya hatua hizo si kwa ajili ya mwanadamu? Ni nani awezaye kuujua moyo wa Mungu, ambao ni sawa na mama mwenye mapenzi? Ni nani awezaye kuujua moyo wa Mungu wenye shauku? Moyo wa upendo na matarajio ya shauku ya Mungu vimelipwa kwa mioyo ya baridi, na usugu, na macho yanayoonyesha kutojali, kwa makaripio ya kujirudia na matusi ya mwanadamu, kwa maneno ya mkato na dhihaka na udhalilishaji, vimelipwa kwa dhihaka ya mwanadamu, kwa kukanyagwa na kukataliwa, kwa kutokuwa na ufahamu, na kupiga kite, na farakano, na uepukaji, kwa uongo, mashambulizi na ukali. Maneno ya wema ya Mungu yamekutana na nyuso kali na ufidhuli wa vidole elfu moja vinavyotikisika. Mungu anaweza tu kustahimili, Akiwa Ameinamisha kichwa, Akiwahudumia watu kama ng'ombe aliye radhi kufungwa.^[2] Miezi na jua nyingi sana, Amekabiliana na nyota mara nyingi sana, Ameondoka alfajiri na kurudi jioni mara nyingi sana, na kurushwarushwa na kugeuzwa, Akivumilia maumivu makubwa mara elfu moja kuliko maumivu Aliyoyapata Alipokuwa Anaondoka kwa Baba Yake, Akivumilia mashambulizi na “kuvunja” kwa mwanadamu, na “kumshughulikia” na “kumpogoa” mwanadamu. Unyenyekevu na kufichika kwa Mungu vimelipwa kwa upendeleo^[3] wa mwanadamu, kwa mitazamo na vitendo vya mwanadamu visivyokuwa vya haki, na kutojulikana Kwake, ustahimilivu, na uvumilivu vimelipizwa kwa jicho la tamaa la mwanadamu, mwanadamu hujaribu kumkanyaga Mungu hadi afe, bila majuto, na anajaribu kumkanyagia Mungu ardhini. Mtazamo wa mwanadamu kwa namna anavyomtendea Mungu ni wa “ujanja adimu,” na Mungu ambaye Anachokozwa na kutwezwa na mwanadamu, Anakanyagwa na kuwa bapa kwa miguu ya makumi elfu ya watu wakati mwanadamu mwenyewe anasimama juu kabisa, kana kwamba angeweza kuwa “mfalme wa kasri,” kana kwamba anataka kuchukua mamlaka kamili,^[4] “kuendesha mahakama akiwa nyuma ya skrini,” kumfanya Mungu kuwa makini na mwenye kanuni “mwongozaji nyuma ya matukio,” ambaye haruhusiwi kupigana au kusababisha shida; lazima Mungu achukue nafasi ya “Mtawala wa Mwisho,” ni lazima Awe “kibaraka,”^[5] bila uhuru wote. Matendo ya mwanadamu hayasemekiki, sasa ana sifa gani ya kutaka hili au lile kuhusu Mungu? Ana sifa gani ya kutoa mapendekezo kwa Mungu? Anafaa kwa kiasi gani kumtaka Mungu amhurumie juu ya udhaifu wake? Anafaa kwa kiasi gani kupokea huruma ya Mungu? Anafaa kwa kiasi gani kupokea ukarimu wa Mungu kila mara? Anafaa kwa kiasi gani kupokea msamaha wa Mungu kila mara? Dhamiri yake ipo wapi? Alivunja moyo wa Mungu muda mrefu uliopita, ni muda mrefu toka

ameuacha moyo wa Mungu katika vipande. Mungu alikuja miongoni mwa wanadamu Akiwa na nguvu nyingi na mwenye shauku kubwa, Akitegemea kwamba mwanadamu atakuwa mkarimu Kwake, hata kama ni kwa wema kiasi kidogo tu. Bado moyo wa Mungu haujafarijiwa na mwanadamu, yote Aliyoyapokea ni mashambulizi na mateso ya kuongezeka haraka;^[6] moyo wa mwanadamu ni wenye tamaa sana, tamaa yake ni kubwa sana, hawezi akatosheka, siku zote ni mwenye fitina na jasiri pasi busara, hawezi kamwe kumpatia Mungu uhuru au haki ya kuzungumza, na anamwacha Mungu bila budi ila kukubali unyanyasaji, na kumruhusu mwanadamu kumtawala vyovyote apendavyo.

Tangu uumbaji hadi leo, Mungu amestahimili maumivu mengi sana, na kupata mashambulizi mengi sana. Ihali hata leo, bado mwanadamu hayalegezi matakwa yake kwa Mungu kwa urahisi, bado anamchunguza Mungu, bado hana uvumilivu Naye, na anachofanya ni kumpatia “ushauri,” na “kumkosoa,” na “kumfundisha nidhamu” kana kwamba Mungu atapotoka njia, kwamba Mungu duniani ni hayawani na Hana busara, au Atafanya fujo, au kwamba Hatafanya kitu chochote cha maana. Mwanadamu siku zote huwa na mtazamo wa aina hii kwa Mungu. Inawezekanaje isimhuzunishe Mungu? Kwa kuwa mwili, Mungu amevumilia maumivu na mateso mengi; ni vibaya kiasi gani, kumfanya Mungu akubali mafundisho ya mwanadamu? Kuwasili kwake miongoni mwa wanadamu kumemvua uhuru wote, kama vile Amefungwa Kuzimu, na Amekubali “uchunguzi” wa mwanadamu bila upinzani hata kidogo. Hii sio aibu? Katika kuja miongoni mwa familia ya wanadamu wa kawaida, “Yesu” amepitia uonevu mkubwa. Na kinachoumiza zaidi ni kwamba Amekuja katika ulimwengu huu wa vumbi na kujinyenyekeza Mwenyewe katika hadhi ya chini kabisa, na Amechukua mwili wa kawaida kabisa. Kwa binadamu kuwa mwembamba, je, Mungu Mwenyezi hapati shida? Na, je, Yeye hafanyi hivyo kwa ajili ya binadamu? Kuna wakati wowote ambapo alikuwa Anajifikiria Mwenyewe? Baada ya kukataliwa na kuuawa na Wayahudi, na kukejeliwa na kudhihakiwa na watu, Hajawahi kulalamika mbinguni au kupinga duniani. Leo, janga hili lenye umri wa milenia limetokea tena miongoni mwa watu hawa wanaofanana na Wayahudi. Je, hawafanyi dhambi ile ile? Nini kinamfanya mwanadamu kuwa na sifa ya kupokea ahadi za Mungu? Je, hampingi Mungu na kisha kukubali baraka Zake? Kwa nini haifikii haki, au kutafuta ukweli? Kwa nini havutiwi na kile ambacho Mungu anafanya? Haki yake iko wapi? Usawa wake uko wapi? Je, ana ujasiri wa kumwakilisha Mungu? Ziko wapi fahamu zake za haki? Ni kiasi gani ambacho kile kinachopendwa na mwanadamu ndicho kile kinachopendwa na Mungu? Mwanadamu hawezi kutambua tofauti muhimu,^[7] siku zote anachanganya kati ya nyeusi na nyeupe,^[8] anakandamiza haki na ukweli, na anashikilia kutokuwa na haki wala usawa kwa kiwango kikubwa. Anafukuzia mbali mwanga na anarukaruka gizani. Wale wanaotafuta ukweli na haki badala yake wanafukuza mwanga, wale wanaomtafuta Mungu wanamkanyaga kwa miguu yao, na wanajipandisha angani.

Mwanadamu hana tofauti na gaidi.^[9] Sababu yake iko wapi? Nani anaweza kutofautisha kati ya jema na baya? Nani anaweza kushikilia haki? Nani yuko tayari kuteseka kwa ajili ya ukweli? Watu ni waovu na wana tabia za kishetani kabisa! Baada ya kumwangika Mungu msalabani wanapiga makofi na kufurahi, vilio vyao havikomi. Wako kama kuku na mbwa, wanashirikiana na kula njama, wameanzisha ufalme wao, udukuzi wao haujaachwa bila kusumbuliwa, wanafumba macho yao na kulia kwa maumivu makali zaidi na zaidi, wote wameungana pamoja, na hali ya kuvurugika imeenea kote, ni harakaharaka na hai, na wale ambao wanajishikamanisha kwa wengine kijinga wanazidi kuibuka, wote wakiwa wameshikilia majina “mashuhuri” ya mababu zao. Hawa mbwa na kuku wamemweka Mungu mbali na akili zao, na hawajawahi kuzingatia kabisa hali ya moyo wa Mungu. Si ajabu kwamba Mungu anasema mwanadamu ni kama mbwa au kuku, mbwa anayebweka anayewafanya mia wengine kutoa mlio mkali; kwa nia hii, kwa makelele mengi ameileta kazi ya Mungu katika siku ya leo, bila kujali kazi ya Mungu ni ya namna gani, bila kujali kuna haki, bila kujali Mungu ana nafasi Yake ya kuweka miguu Yake, bila kujali kesho itakuwaje, uduni wake, na hali yake ya kuwa mchafu. Mwanadamu hajawahi kufikiria juu ya mambo kiasi hicho, hajawahi kuhofia kesho, na amekusanya yale yote ambayo ni ya manufaa na ya thamani na kuyakumbatia, na bila kumwachia Mungu chochote isipokuwa mabaki na makombo.^[10] Binadamu ni katili kiasi gani! Hana hisia hata kidogo kwa Mungu, na baada ya kuteketeza kila kitu cha Mungu, anamrusha Mungu nyuma yake na kuacha kujali kabisa kuhusu uwepo wake. Anamfurahia Mungu, halafu anampinga Mungu, na anamkanyagia chini ya miguu yake, wakati mdomoni mwake anamshukuru na kumsifu Mungu; anamwomba Mungu, na anamtegemea Mungu, wakati huo pia anamdanganya Mungu; “analiinua” jina la Mungu, na kuutazama uso wa Mungu, halafu pia bila haya na bila kuwa na aibu anakaa katika kiti cha enzi cha Mungu na “kuhukumu” “udhalimu” wa Mungu; kutoka katika kinywa chake yanatoka maneno haya “anapaswa kumshukuru Mungu,” na anatazama katika maneno ya Mungu, halafu katika moyo wake anavurumisha shutuma kwa Mungu; ni “mvumilivu” kwa Mungu halafu anamkandamiza Mungu, na kinywa chake kinasema ni “kwa ajili ya Mungu”; mikononi mwake ameshikilia vitu vya Mungu, na kinywani mwake anatafuna chakula ambacho Mungu amempatia, bado macho yake yanamtazama Mungu yakiwa hayana hisia kabisa, kana kwamba anatamani kummeza; anautazama ukweli lakini anasisitiza kuwa ni hila za Shetani; anatazama haki lakini analazimisha iwe kujikana nafsi; anatazama matendo ya mwanadamu lakini anasisitiza kuwa ni kile Mungu alicheo; anatazama karama za asili za mwanadamu lakini anasisitiza kuwa ni ukweli; anatazama matendo ya Mungu lakini anasisitiza kuwa ni kiburi na majivuno, majigambo na haki binafsi; mwanadamu anapomwangalia Mungu anasisitiza kumpachika uanadamu, na anajitahidi sana kumweka katika kiti cha kiumbe aliyeumbwa akishirikiana na Shetani; anajua kweli kabisa ni matamshi ya Mungu, bado atasema si kitu chochote zaidi ya maandiko ya mwanadamu; anajua kabisa kwamba Roho anatabulika katika

mwili, kwamba Mungu amekuwa mwili, lakini anasema mwili huu ni uzao wa Shetani; anajua kikamilifu kuwa Mungu ni mnyenyekevu na hajionyeshi, lakini anasema kwamba Shetani ameaibishwa na Mungu ameshinda. Uzuri wa bure ulioje! Mwanadamu hata hafai kuwa mbwa mlinzi! Hawezi kutofautisha kati ya nyeusi na nyeupe, na hata anachanganya kwa makusudi nyeusi ndani ya nyeupe. Je, nguvu za mwanadamu na husuru ya mwanadamu vinaweza kustahimili siku ya ukombozi wa Mungu? Baada ya kumpinga Mungu kwa kukusudia, mwanadamu hakuweza kujali sana, au hata kwenda mbali sana na kumuua, asimpatie Mungu nafasi ya kujionyesha Mwenyewe. Haki iko wapi? Upendo uko wapi? Anakaa kando ya Mungu na kumsukuma Mungu apige magoti ili Aombe msamaha, kutii mipango yake yote, kuridhia hila zake zote, na anamfanya Mungu kuchukua ishara Zake zote kutoka Kwake, la sivyo anaghadhibishwa^[11] na kupandwa na hasira. Inawezekanaje Mungu asiwe na maumivu katika ushawishi huo wa giza, ambao unachanganya nyeusi kuwa nyeupe? Angewezaje kukosa kuwa na wasiwasi? Kwa nini inasemwa kwamba Mungu alipoanza kazi Yake ya hivi karibuni kabisa, ilikuwa ni kama kazi ya kuumba mbingu na dunia? Matendo ya mwanadamu “yana utajiri,” ni “chemchemi isiyokoma ya maji ya uzima” bila kukoma “yanajaza tena” shamba la moyo wa mwanadamu, wakati “chemchemi isiyokoma ya maji ya uzima” ya mwanadamu “inashindana” na Mungu bila haya;^[12] wawili hawa hawapatani, na anawapa watu vitu kwa niaba ya Mungu bila hofu ya kuadhibiwa wala kuumia, wakati mwanadamu anashirikiana naye bila kujali hatari iliyopo. Na kwa athari gani? Anamtupilia mbali Mungu upande mmoja, na kumweka mbali sana, ambapo watu hawatamzingatia, akiogopa sana kwamba Atavuta usikivu wake, na anaogopa sana kwamba chemchemi isiyokoma ya maji ya uzima ya Mungu itamteka mwanadamu, na kumpata mwanadamu. Hivyo, baada ya kupitia uzoefu wa miaka mingi wa masuala ya kidunia, anakula njama dhidi ya Mungu, na hata anamfanya Mungu kuwa mlengwa wa “adhabu.” Ni kana kwamba Mungu amekuwa gogo machoni mwake, na anatamani kumnyakua Mungu na kumweka motoni ili Atakaswe na kusafishwa. Mwanadamu anapooni mahangaiko ya Mungu, anapiga kifua chake na kucheka, anacheza kwa furaha, na kusema kwamba Mungu pia Amewekwa motoni, na anasema kwamba atausafisha uchafu wa Mungu, kana kwamba hili ni la urazini na lina maana, kana kwamba hizi tu ndizo njia za haki na zenye mantiki za Mbinguni. Tabia hii ya fujo ya mwanadamu inaonekana kuwa ni ya makusudi na ya kutofahamu. Mwanadamu anafichua uso wake mbaya na roho yake mbaya, vilevile sura ya kusikitisha ya ombaomba; baada ya kufanya ghasia sana, anavaa sura ya kuhurumiwa na kuomba msamaha wa Mbingu, akifanana na udongo wa kufinyangwa. Mwanadamu siku zote hutenda kwa namna asiyotarajiwa, siku zote “anamwendesha duma kuwatisha wengine,”^[a] yeye daima huwa akiigiza sehemu fulani, hajali hata kidogo moyo wa Mungu, wala halinganishi hadhi yake mwenyewe. Kimyakimya anampinga Mungu, kana kwamba Mungu amemkosea, na Hapaswi kumtendea hivyo, na kana kwamba Mbingu haina macho na inafanya kwa makusudi mambo kuwa magumu kwake. Hivyo

mwanadamu anapanga njama za siri, na hajali matakwa ya Mungu hata kidogo, anatazama kwa macho ya mnyama mkali, anatazama kwa hasira kila kitu Anachokifanya Mungu, hafikirii kwamba yeye ni adui ya Mungu, na ana matumaini kwamba siku itakuja ambapo Mungu atautawanya umande na kuviweka vitu wazi, na kumwokoia kutoka katika “kinywa cha duma” na kulipiza kisasa kwa niaba yake. Hata leo, watu bado hawafikiri kwamba wanatekeleza jukumu la kumpinga Mungu, jukumu ambalo limefanywa kwa enzi nyingi sana, wangeweza kujua kwamba, katika yote wanayofanya, wamepotoka tangu zamani sana, kwamba yote waliyoyaelewa yamemezwa na bahari zamani sana.

Ni nani amewahi kukubali ukweli? Ni nani amewahi kumkaribisha Mungu kwa mikono yote? Nani amewahi kutamani uwepo wa Mungu? Tabia ya mwanadamu imeoza tangu zamani sana, na unajisi wake umefanya hekalu la Mungu lisitambulike tangu zamani sana. Mwanadamu, wakati akiendelea kufanya kazi yake, amekuwa akimdharau Mungu. Ni kana kwamba upinzani wake kwa Mungu umeandikwa kwenye jiwe, na haubadiliki, na matokeo yake ni bora alaniwe kuliko kuendelea kuteseka “kwa kufanyiwa vibaya” na maneno na matendo yake. Inakuwaje watu kama hawa wamjue Mungu? Wanawezaje kupata pumziko kwa Mungu? Na wanawezaje kufaa kuja mbele za Mungu? Bila shaka, hakuna chochote kibaya kujitoa kwa mpango wa usimamizi wa Mungu—lakini kwa nini watu daima huweka kazi ya Mungu na ukamilifu wa Mungu akilini mwao huku wakitoa kwa dhati damu na machozi yao wenyewe? Roho ya watu ya kujitokea kwa dhati, bila shaka, ni ya thamani—lakini wangejua kwamba “hariri” wanayoisokota haiwezi kabisa kuwakilisha kile Mungu aliche? Nia nzuri za watu, bila shaka, ni za thamani na adimu—lakini wangeweza kumeza “hazina ya thamani mno”?^[13] Kila mmoja wenu anapaswa kufikiria juu ya maisha yenu ya zamani: Kwa nini hamjawahi kuwa mbali na kuadibu na laana ya kikatili? Kwa nini watu daima “huwa na uhusiano wa karibu” na maneno adhimu na hukumu yenye haki? Je, Mungu anawajaribu kwa kweli? Je, Mungu anawasafisha kwa makusudi? Na watu huingiaje katikati ya usafishaji? Je, wanajua kazi ya Mungu kweli? Ni mafunzo gani ambayo watu wamejifunza kutoka kwa kazi ya Mungu na kuingia kwao wenyewe? Watu wasisahau kusihi kwa Mungu, na wawe na ufahamu katika kazi ya Mungu, waitambue kwa uwazi kabisa, na kusimamia vizuri kuingia kwao wenyewe.

Tanbihi:

1. “Maangamizi” inatumiwa kuweka wazi kutotii kwa wanadamu.
2. “Anaweza tu kustahimili, Akiwa Ameinamisha kichwa, Akiwahudumia watu kama ng’ombe aliye radhi kufungwa” ni kwa asili sentensi moja, lakini hapa imegawanywa mara mbili ili kuyafanya mambo wazi zaidi. Sentensi ya kwanza inahusu matendo ya mwanadamu, huku ya pili inaonyesha mateso aliyoyapitia Mungu, na kwamba Mungu ni mnyenyekevu na Aliyefichika.
3. “Upendeleo” unahusu tabia ya watu ya ukaidi.

4. “Kuchukua mamlaka kamili” inahusu tabia ya watu ya ukaidi. Wanajitukuza, huwafunga wengine, wakiwafanya wawafuate na kuteseka kwa ajili yao. Wao ni majeshi ambayo ni ya uadui kwa Mungu.

5. “Kibaraka” inatumiwa kuwadhihaki wale ambao hawamjui Mungu.

6. “Kuongezeka haraka” inatumiwa kuonyesha tabia duni ya watu.

7. “Hawezi kutambua tofauti muhimu” inaonyesha wakati ambapo watu wanageuza mapenzi ya Mungu kuwa kitu cha kishetani, ikitaja kwa upana tabia ambayo kwayo watu humkataa Mungu.

8. “Anachanganya kati ya nyeusi na nyeupe” inahusisha kuchanganya ukweli na njozi, na haki na uovu.

9. “Gaidi” inatumiwa kuonyesha kwamba watu ni wapumbavu na hawana ufahamu.

10. “Mabaki na makombo” inatumiwa kuonyesha tabia ambazo kwazo watu humdhulumu Mungu.

11. “Anaghadhibishwa” inahusu uso mbaya wa mwanadamu aliye na hasira na aliyeudhika.

12. “Bila haya” inahusu wakati ambapo watu hawajali, na hawana uchaji kuhusiana na Mungu hata kidogo.

13. “Hazina ya thamani mno” inahusu ukamilifu wa Mungu.

a. Hili limetafsiriwa kulingana na maandishi asili “hú jiǎ hǔ wēi”, ambayo ni msemo wa Kichina. Yanarejelea hadithi ambamo mbweha anawafukuza wanyama wengine kwa kutembea kama pamoja na chui mwenye milia, hivyo “kuazima” hofu na hadhi ambayo chui mwenye milia anaibua. Hii ni istiaira, inayotumiwa hapa kuashiria watu “wanaoazima” hadhi ya mtu mwingine ili kuwaogofya au kuwadhulumu watu wengine.

Kazi na Kuingia (10)

Kwa wanadamu kuendelea mbele kiasi hiki ni hali isiyo na kigezo. Kazi ya Mungu na kuingia kwa mwanadamu vinaendelea bega kwa bega, na hivyo kazi ya Mungu, pia, ni tukio kubwa lisilo na kifani. Kuingia kwa mwanadamu hadi sasa ni ajabu ambayo kamwe haijawahi kufikiriwa na mwanadamu. Kazi ya Mungu imefikia upeo wake—na, kufuatia, “kuingia” kwa mwanadamu^[1] pia kumefikia kilele chake. Mungu amejishusha kwa kadiri Anavyoweza, na kamwe Hajawahi kuwalalamikia wanadamu au kwa ulimwengu na vitu vyote. Mwanadamu, wakati ule ule, anasimama juu ya kichwa cha Mungu, akimnyanyasa hadi kilele; yote yamefikia kilele chake, ni wakati wa siku ambapo haki inaonekana. Kwa nini uendeleo kuacha huzuni iifunike nchi, na giza kuwavaa watu wote? Mungu ameangalia kwa miaka elfu kadhaa—kwa makumi ya maelfu ya miaka, hata—na uvumilivu Wake umekwisha kufikia kikomo chake. Amekuwa akiangalia kila hatua za wanadamu, Amekuwa akiangalia kwa makini jinsi udhalimu wa mwanadamu utafanya fujo, na bado mwanadamu, ambaye amekuwa wa kutojali kwa muda mrefu, hahisi chochote. Na ni nani aliyewahi kuangalia kwa makini matendo ya Mungu? Nani aliyewahi kuinua macho yake na kutazama mbali sana? Nani aliyewahi kusikiliza kwa makini? Nani aliyewahi kuwa mikononi mwa Mwenyezi? Watu wote wanakerwa na hofu za kubuni^[2]. Je, kuna faida gani kwa rundo la nyasi kavu na majani makavu? Kitu pekee wanachoweza kufanya ni kumtesa Mungumwenye mwili hadi kifo. Ingawa wao ni mafungu tu ya nyasi kavu na majani makavu, bado kuna kitu

kimoja ambacho wao hufanya “bora zaidi”:^[3] kumtesa Mungu hadi kifo na kisha kulia kwamba “hilo hufurahisha mioyo ya watu.” Kikundi cha jeshi lisilofaa kabisa! La ajabu, katikati ya mkondo usiokwisha wa watu, wao hulenga uangalifu wao juu ya Mungu, wakimzunguka Yeye na zingio lisilopenyeka. Hamasa yao daima ikiwaka moto zaidi,^[4] wamemzunguka Mungu katika vikundi, ili Asiweze kusonga hata kidogo. Katika mikono yao, wanashikilia kila aina ya silaha, na kumtazama Mungu kana kwamba wanamwanguka adui, macho yao yakiwa yamejaa hasira; wana hamu ya “kumshambulia Mungu kwa nguvu.” Inafaidi kweli: Kwa nini mwanadamu na Mungu wamekuwa maadui wasioweza kupatanishwa? Inawezekana kwamba kuna chuki ya muda mrefu sana kati ya Mungu wa upendo sana na mwanadamu? Inawezekana kwamba matendo ya Mungu hayana faida kwa mwanadamu? Je, hayo humdhuru mwanadamu? Mtu hulenga jicho la hasira lisiloyumba juu ya Mungu, akiogopa sana kwamba Atapasua zingio la mwanadamu, Arudi mpaka mbingu ya tatu, na mara nyingine tena Amtupe mwanadamu ndani ya gereza. Mwanadamu anajihadhari na Mungu, yeye ni mwenye wasiwasi, na hufurukuta toka upande mmoja hadi upande mwingine wa ardhi kwa mbali, akishikilia “bombomu” ambayo inamlenga Mungu kati ya wanadamu. Ni kana kwamba, Mungu akijitikisa kidogo tu, mwanadamu atafuta kila kitu Chake—mwili Wake wote na yote Anayovaa—bila kuacha kitu chochote. Uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu hauwezi kurekebisha. Mungu haeleweki kwa mwanadamu; mwanadamu, wakati ule ule, huyafunga macho yake kwa makusudi na kucheza, asiyetaka kabisa kuona kuwepo Kwangu, na kutosamehe hukumu Yangu. Hivyo, wakati mtu hatarajii, Mimi huondoka kimya kimya, na Sitaweza tena kulinganisha nani aliye juu na nani aliye chini na mwanadamu. Wanadamu ni “wanyama” wa chini zaidi kuliko wote na Sitamani kumsikiliza tena. Kwa muda mrefu Nimerudisha neema Yangu yote mahali ambapo Mimi hukaa kwa amani; kwa kuwa mwanadamu ni mkaidi sana, ana sababu gani kufurahia zaidi neema Yangu ya thamani mno? Mimi siko tayari kutoa neema Yangu bure juu ya nguvu zilizo na uhasama Kwangu. Ningetoa matunda Yangu ya thamani juu ya wale wakulima wa Kanaani ambao ni wenye ari, na wanakaribisha kwa dhati kurudi Kwangu. Napenda tu mbingu ziendelee milele, na, zaidi ya hayo, mwanadamu asizeeke kamwe, mbingu na mwanadamu viwe vitulivu daima, na ile “misonobari na mivinje” iliyo na rangi ya kijani daima iandamane na Mungu, na daima iandamane na mbingu katika kuingia kwenye enzi kamilifu pamoja.

Nimetumia siku nyingi kuwa na mwanadamu, Nimeishi duniani pamoja na mwanadamu, na Sijawahi kutaka vitu zaidi kutoka kwa mwanadamu, Ninamwongoza tu mwanadamu kusonga mbele, Sifanyi chochote bali kumwongoza mwanadamu, na kwa ajili ya hatima ya binadamu, bila kuchoka Nafanya kazi ya kupangilia. Nani ambaye amewahi kuelewa mapenzi ya Baba wa mbinguni? Nani amewahi kusafiri kati ya mbingu na dunia? Sitamani kuishi tena na mwanadamu katika “uzee” wake, kwani mwanadamu ni “wa mtindo wa zamani sana,” hajui chochote; kitu

pekee anachojua ni kula na kuvimbiwa kwenye sherehe Niliyoandaa, amejitenga na yote, hafikirii suala jingine lolote lile. Binadamu anateseka sana, makelele, huzuni, na hatari miongoni mwa wanadamu ni kubwa sana, na hivyo Natamani nisiwashirikishe matunda ya thamani ya kupata ushindi wakati wa siku za mwisho. Acha mwanadamu afurahie baraka tele ambazo ametengeneza mwenyewe, maana mwanadamu hanikaribishi—kwa nini Nimshurutishe binadamu kulazimisha tabasamu? Kila pembe ya dunia haina joto, hakuna hata chembe ya chemchemi katika ardhi yote ya nchi, maana, hana joto hata kidogo kama mnyama aishiye majini, ni kama maiti, na hata damu inayopita katika mishipa yake ni kama barafu iliyoganda inayofanya moyo kuwa baridi. Wema upo wapi? Mwanadamu alimsulubisha Mungu msalabani bila sababu yoyote, na baadaye hakuhihi wasiwasi wowote. Hakuna hata mmoja aliyekuwa na majuto, na madikteta hawa makatili bado wanapanga “kumkamata Akiwa hai”^[5] Mwana wa Adamu kwa mara nyingine na kumleta mbele ya kikosi cha kufyatua risasi, kukomesha chuki ndani ya mioyo yao. Kuna faida gani Kwangu, kubaki katika nchi hii ya hatari? Ikiwa Nitabaki, kitu pekee Nitakachomletea mwanadamu ni mgogoro na fujo, na hakutakuwa na mwisho wa shida, maana Sijawahi kumpatia mwanadamu amani, ni vita tu. Siku za mwisho za binadamu lazima zijae vita, na hatima ya mwanadamu lazima ipinduliwe katikati ya vurugu na migogoro. Na Sipo tayari kushiriki katika “furaha” ya vita, Sitaunga mkono umwagaji wa damu na mwanadamu kujitoa mhanga, maana kukataliwa na mwanadamu kumenipeleka katika hali ya kukata tamaa, na Sina moyo wa kuangalia vita vya mwanadamu—hebu mwanadamu apigane kuuridhisha moyo wake, Natamani kupumzika, Nataka kulala, acha mapepo wawe washirika wa binadamu wakati wa siku zao za mwisho! Nani ajuaye mapenzi Yangu? Kwa sababu Sijakaribishwa na mwanadamu, na hajawahi kunisubiri, Ninaweza tu kumuaga, na kumkabidhi hatima yake, na kumwachia mwanadamu utajiri Wangu wote, na kupanda maisha Yangu ndani yake, kupanda mbegu ya maisha Yangu ndani ya shamba la moyo wa mwanadamu, na kumwachia kumbukumbu za milele, Ninaweza kuacha tu upendo Wangu wote kwa binadamu, kumwachia yote ambayo mwanadamu anafurahia Kwangu, kama zawadi ya upendo ambayo tunaitamani iwe kwa kila mmoja. Ningependa tupendane milele, kwamba jana yetu iwe kitu kizuri sana tunachopeana, maana Nimejitoe kikamilifu kwa binadamu—ni malalamiko gani ambayo mwanadamu anaweza kuwa nayo? Tayari Nimeyaacha maisha Yangu yote kwa mwanadamu, na bila neno lolote, Nimetokwa jasho kwa kulima “ardhi nzuri ya upendo” kwa ajili ya binadamu; Sijafanya matakwa yoyote linganifu kwa mwanadamu, na Sijafanya chochote isipokuwa kujitiisha katika mipangilio ya mwanadamu na kutengeneza kesho nzuri zaidi ya binadamu.

Ingawa kazi ya Mungu ni yenye ukwasi na maridhawa, kuingia kwa mwanadamu kuna upungufu sana. Kwa “shughuli” ya pamoja kati ya mwanadamu na Mungu, karibu yote ni kazi ya Mungu;

kuhusu kiasi gani mwanadamu ameingia, hana ushahidi wa chochote alichopata Mwanadamu, ambaye amechakaa sana na ni kipofu, hata hutathmini nguvu zake dhidi ya Mungu wa leo na “silaha za kale” mikononi mwake. Hawa “sokwe wa kale” huweza kutembea wima kwa shida, na hawaoni aibu katika miili yao iliyo “uchi.” Ni nini kinawastahilisha kutathmini kazi ya Mungu? Macho ya wengi wa sokwe hawa wa miguu minne hujaa ghadhabu, nao hujipambanisha na Mungu kwa silaha za kale za mawe mikononi mwao, wakijaribu kuanzisha mashindano ya sokwe watu ambao dunia haijawahi kuwaona kamwe hapo awali, kuwa na mashindano ya siku za mwisho kati ya sokwe watu na Mungu ambayo yatakuwa maarufu duniani kote. Wengi wa sokwe watu hawa walio nusu wima, zaidi ya hayo, hufurikwa na ridhaa. Nywele zikiwa zimefunika nyuso zao zilizofungamana, wamejaa nia ya kuua na huinua miguu yao ya mbele. Bado hawajageuka kwa ukamilifu kuwa mtu wa kisasa, kwa hiyo wakati mwingine wao husimama wima, na wakati mwingine wao hutambaa, shanga za jasho zikifunika paji la nyuso zao kama matone ya umande yaliyo karibu karibu, hamu yao ni dhahiri. Ukimwanguka sokwe mtu, wa asili, rafiki yake, akiwa amesimama kwa miguu yote minne, miguu yake minne ikiwa mikubwa na ya mwendo wa polepole, inayoweza kukwepa mapigo kwa shida na bila nguvu ya kupigana, anajizuia kwa shida. Kufumba na kufumbua—kabla ya kuwa na wakati wa kuona nini kilichotokea—“shujaa” katika ulingo huanguka chini ghafula, miguu ikiwa hewani. Miguu hiyo, iliyokaa vibaya juu ya ardhi kwa miaka yote hiyo, ghafula imegeuzwa juu chini, na sokwe mtu huyo hana tena hamu ya kupinga. Kuanzia wakati huu kuendelea, sokwe mtu kati ya sokwe watu wa kale zaidi anaondolewa kutoka kwenye uso wa dunia—ni la “kuhuzunisha” kweli. Huyu sokwe mtu wa kale alifikia mwisho wa ghafla. Kwa nini alikuwa na haraka kutoka katika ulimwengu wa ajabu wa mwanadamu mapema hivyo? Kwa nini hakuzungumzia hatua inayofuata ya mkakati na wenzake? Inasikitisha kwamba aliuaga ulimwengu bila kuacha siri ya kutathmini nguvu za mtu dhidi ya Mungu! Haikuwa busara kwa sokwe mtu huyo mzee kufa bila kunong’ona, kuondoka bila kupitisha “utamaduni wa kale na sanaa” kwa dhuria zake. Hakukuwa na wakati wa kuwaita wale walio karibu naye ubavuni mwake kuwaambia juu ya upendo wake, hakuacha ujumbe juu ya kibao cha mawe cha kuandikia, hakutambua jua la mbingu, wala haku sema chochote juu ya shida zake zisizoweza kuzungumziwa. Alipokuwa akipumua pumzi yake ya mwisho, hakuwaita wazao wake ubavuni pa mwili wake uliokuwa ukifa kuwaambia “msiingie ndani ya ulingo ili kumpinga Mungu” kabla ya kufumba macho yake, miguu minne migumu ikijitokeza juu daima kama matawi ya mti ikielekeza angani. Ingeonekana alikufa kifo cha uchungu.... Ghafla, kicheko cha kunguruma kinafoka kutoka chini ya ulingo; mmoja wa sokwe watu aliye nusu wima aliyejizuzua; akiwa ameshika “kigongo cha mawe” cha kuwinda paa au wanyama wengine wa mwitu kilichoendelea zaidi kuliko kile cha sokwe mtu wa kale, anaruka ndani ya ulingo, akiwa amejawa na hasira, akiwa na mpango alioufikiria kwa makini katika akili yake.^[6] Ni kana kwamba amefanya kitu chenye kustahili. Kwa kutumia “nguvu” ya

kigongo chake cha mawe anafanikiwa kusimama wima kwa “dakika tatu.” Ajabu jinsi “nguvu” ya huu “mguu” wa tatu ilivyo kuu! Alimshikilia sokwe mtu mkubwa, goigoi, mpumbavu aliye nusu wima akisimama kwa dakika tatu—si ajabu sokwe mtu huyu mzee wa kuheshimiwa^[7] ni jeuri sana. Kwa kweli, kifaa cha jiwe cha kale “kilikuwa kizuri kama sifa zake”: Kuna mpini wa kisu, makali, na ncha, dosari pekee ni ukosefu wa mng’aro kuelekea ukingo—jinsi hilo linavyosikitisha. Tazama tena “shujaa mdogo” wa nyakati za kale, aliyesimama ulingoni akiwaangalia wale walio chini na kuwakazia macho kwa dharau, kana kwamba wao ni wadhaifu walio duni, na yeye ni shujaa hodari. Katika moyo wake, anawachukia kwa siri wale walio mbele ya jukwaa. “Nchi iko taabani na kila mmoja wetu anawajibika, kwa nini mnaepa? Inawezekana kuwa ninyi mnaona nchi inakabiliwa na maangamizi, lakini hamshiriki katika vita vikali? Nchi inakaribia kuangamizwa—kwa nini ninyi sio wa kwanza kushughulika, na wa mwisho kujifurahisha? Mnawezaje kusimama na kuiangalia nchi ikianguka na watu wake wakianguka katika uozo? Je, mko tayari kubeba aibu ya kutiishwa kwa taifa? Kikundi cha vinyangarika kweli!” Anapofikiria hili, ghasia zinatokea mbele ya jukwaa na macho yake yanakasirishwa hata zaidi, kana kwamba karibu kutupa^[8] miale. Ana hamu ya Mungu kushindwa kabla ya vita, akiwa tayari kufanya lolote kumuua Mungu ili awafurahishe watu. Hajui hata kidogo kwamba, ingawa kifaa chake cha jiwe kinaweza kuwa cha sifa inayostahili, hakiwezi kamwe kumchokoza Mungu. Kabla hajapata wakati wa kujikinga, kabla hajapata wakati wa kulala chini na kusimama, anayumba nyuma na mbele, uwezo wa kuona umepotea kutoka kwa macho yote. Anaanguka chini ghafula kwa babu yake wa zamani na hainuki tena; akimshikilia kwa nguvu sokwe mtu wa kale, halii tena, na anakubali udhalili wake, hana tena tamaa yoyote ya kupinga. Sokwe watu hao wawili maskini wanakufa mbele ya ulingo. Ni jambo la kusikitisha kwamba mababu za wanadamu, ambao wamenusurika hadi siku hii, walikufa kijinga katika siku ambayo Jua la haki lilionekana! Ni upumbavu ulioje kuwa wameiacha baraka kubwa sana kama hiyo kuwapita—kwamba, katika siku ya baraka yao, sokwe watu ambao wamengoja kwa maelfu ya miaka wamepeleka baraka Kuzimu ili “kufurahia” na mfalme wa pepo! Kwa nini wasiweke baraka hizi katika ulimwengu wa walio hai ili wafurahie na wana na binti zao? Wanatafuta tu shida! Huku ni kupoteza tu kwamba, kwa ajili ya hadhi ndogo, sifa, na ubatili, wanateseka kwa kuchinjwa, kung’ang’ana kuwa wa kwanza kufungua milango ya jahanamu na kuwa wana wake. Gharama kama hiyo si lazima. Inasikitisha mababu wa zamani kama hao, waliokuwa “wamejawa sana na roho ya kitaifa,” wangukuwa “wakali sana kwao wenyewe lakini wenye kuwavumilia wengine sana,” wakijifungia jahanamu, na kuwafungia wale dhaifu walio duni nje. Ni wapi ambako “wawakilishi wa watu” kama hawa wanaweza kupatikana? Kwa ajili ya “ustawi wa uzao wao” na “maisha ya amani ya vizazi vijavyo,” hawamruhusu Mungu kuingilia kati, na hivyo hawatilii maanani maisha yao wenyewe. Bila kujizuia, wanajitolea kwa “kusudi la kitaifa,” kuingia Kuzimu bila kusema lolote. Utaifa kama huo unaweza kupatikana wapi? Wakipigana na Mungu,

hawaogopi kifo, wala kumwaga damu, seuze kuwa na wasiwasi kuhusu kesho. Wanakwenda tu kwenye uwanja wa vita. Inasikitisha kwamba kitu pekee wanachopata kwa “roho yao ya kujitolea” ni majuto ya milele, na kuteketezwa na moto wa kuzimu uwakao milele!

Jinsi inavyovutia! Kwa nini kupata mwili kwa Mungu daima kumekataliwa na kushutumiwa na watu? Kwa nini watu hawawi na ufahamu wowote wa kupata mwili kwa Mungu kamwe? Inawezekana kuwa Mungu amekuja wakati mbaya? Inawezekana kuwa Mungu amekuja mahali pabaya? Inawezekana kwamba hili hutokea kwa sababu Mungu ametenda peke yake, bila “sahihi” ya mwanadamu? Inawezekana ni kwa sababu Mungu alifanya maamuzi Yake Mwenyewe bila ruhusa ya mwanadamu? Ukweli unasema kwamba Mungu alitoa taarifa ya awali. Mungu hakufanya makosa kuwa mwili—je, Anahitaji kuomba idhini ya mwanadamu? Zaidi ya hayo, Mungu alimkumbusha mwanadamu zamani, labda watu wamesahau. Hawapaswi kulaumiwa, kwa kuwa mwanadamu kwa muda mrefu amepotoshwa sana na Shetani kiasi kwamba hawezi kuelewa chochote kinachoendelea chini ya mbingu, sembuse matukio ya ulimwengu wa kiroho! Ni aibu iliyoje kwamba mababu wa mwanadamu, sokwe watu, walikufa katika ulingo, lakini hili halishangazi: Mbingu na dunia hazijawahi kulingana, na ni jinsi gani sokwe watu, ambao akili zao zimetengenezwa kwa mawe, wangeweza kudhani kwamba Mungu angeweza kupata mwili tena? Ni jambo la kusikitisha kwamba “mtu mzee” kama huyu ambaye yuko kwenye “miaka yake ya sitini” alikufa katika siku ya kuonekana kwa Mungu. Je, si jambo la kushangaza kwamba aliuacha ulimwengu bila baraka katika ujio wa baraka kubwa kama hiyo? Hali ya Mungu kupata mwili imesababisha mawimbi mazito katika dini na madhehebu yote, “imeparaganya” mpangilio wa awali wa jamii ya kidini, na imetikisa mioyo ya wale wanaotamani sana kujitokeza kwa Mungu. Ni nani asiyeabudu? Nani hatamani kumwona Mungu? Mungu amekuwa miongoni mwa wanadamu kwa miaka mingi sana, lakini mwanadamu kamwe hajawahi kutambua. Leo, Mungu Mwenyewe amejitokeza, na Ameonyesha utambulisho Wake kwa watu—inawezekanaje hii isiupatie moyo wa mwanadamu furaha? Mungu aliwahi kushiriki furaha na huzuni pamoja na mwanadamu, na leo Ameunganika tena na mwanadamu, na kushiriki visa vya muda uliopita pamoja naye. Baada ya kutoka Uyahudi, watu hawakuweza kupata alama Yake yoyote. Wanatamani kukutana tena na Mungu, bila kujua kwamba leo wamekutana Naye tena, na kuungana Naye tena. Inawezekanaje hii isiamshe mawazo ya jana? Siku kama ya leo miaka elfu mbili iliyopita, Simoni mwana wa Yona, uzao wa Wayahudi, alimtazama Yesu Mwokozi, alikula meza moja pamoja Naye, na baada ya kumfuata kwa miaka mingi alihisi kumpenda sana: Alimpenda sana kwa dhati, alimpenda sana Bwana Yesu. Watu wa Uyahudi hawakujua chochote kuhusu vile mtoto huyu mwenye nywele za dhahabu, Aliyezaliwa katika hori la ng’ombe, Alikuwa ni sura ya kwanza ya Mungu kupata mwili. Wote walidhani kwamba Alikuwa ni mmoja wao, hakuna aliyedhani kwamba Yupo tofauti nao—watu

wangeweze kumtambua Yesu wa desturi na wa kawaida kabisa? Watu wa Uyahudi walidhani kwamba alikuwa ni mtoto wa Kiyahudi wa wakati huo. Hakuna aliyemtazama kama Mungu mwenye upendo, na watu hawakufanya chochote isipokuwa kufanya maombi bila kutambua, wakiomba Awape neema nyingi na maradufu, na amani, na furaha. Walijua tu kwamba, kama milionea, Alikuwa na kila kitu ambacho mtu angetamani kuwa nacho. Lakini watu hawakumchukulia kama mtu ambaye Alikuwa mpendwa; watu wa wakati huo hawakumpenda, na walimpinga tu, na walifanya maombi Kwake yasiyokuwa na mantiki, na Hakuwahi kupinga, Aliendelea kutoa neema kwa mwanadamu, ingawa mwanadamu hakumjua. Hakufanya chochote isipokuwa kwa kimya kumpatia mwanadamu wema, upendo, na huruma, na zaidi, Alimpatia mwanadamu njia mpya ya kutenda, kumwongoza mwanadamu kutoka katika vifungo vya sheria. Mwanadamu hakumpenda, alimhusudu tu na kutambua “talanta Zake za kipekee.” Inawezekanaje mwanadamu kipofu kujua jinsi Yesu Mwokozi alipitia mateso makubwa Alipokuja miongoni mwa wanadamu? Hakuna aliyejali shida Zake, hakuna mtu aliyejua upendo Wake kwa Mungu Baba, na hakuna ambaye angejua upweke Wake; ingawa Maria alikuwa mama Yake wa kumzaa, angeweze kujua mawazo yaliyopo moyoni mwa Bwana Yesu mwenye huruma? Nani alijua mateso yasiyoweza kutamkika Aliyoyapitia Mwana wa Adamu? Baada ya kumwomba watu wa kipindi hicho walimweka nyuma ya akili zao, na kumtupa nje Akizungukazunguka mitaani, siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, na kwenda bila mwelekeo kwa miaka mingi hadi Alipofikisha miaka thelathini na mitatu, miaka ambayo ilikuwa mirefu pia mifupi. Watu walipomhitaji, walimwalika nyumbani mwao wakiwa na nyuso za tabasamu, wakijaribu kumwomba kitu—na baada ya kuwa Ametoa mchango wake kwao, walimsukuma mara moja nje ya mlango. Watu walikula kile Alichokitoa mdomoni Mwake, walikunywa damu Yake, walifurahia neema Aliyowapatia, lakini bado walimpinga, maana hawakujua nani aliwapa uhai walionao. Hatimaye, walimsulubisha msalabani, lakini bado Hakutoa hata sauti. Hata leo, bado Anabakia kimya. Watu wanakula mwili Wake, wanakunywa damu Yake, wanakula chakula Anachowatengenezea, na wanapita njia Aliyofungua kwa ajili yao, lakini bado wanakusudia kumkataa, kimsingi wanamchukulia Mungu ambaye Amewapatia maisha yao kama adui, na badala yake wanawachukulia wale ambao ni watumwa kama wao kama Anavyofanya Baba wa mbinguni. Katika hili, je, hawampingi kwa makusudi? Yesu aliwezaje kufa msalabani? Je, mnajua? Je, Hakusalitiwa na Yuda, ambaye alikuwa karibu kabisa Naye, na akamla, akamnywa, na akamfurahia? Je, Yuda hakumsaliti Yesu kwa sababu Alikuwa tu mwalimu wa kawaida Asiye na umuhimu? Ikiwa watu walikuwa wameona kwamba Yesu alikuwa si wa kawaida kabisa, na Ambaye Alitoka mbinguni, wangeweze kumsulubisha msalabani Akiwa hai kwa masaa ishirini na nne, hadi Alipoishiwa na pumzi yote katika mwili wake? Nani awezaye kumjua Mungu? Watu hawafanyi chochote isipokuwa kumfurahia Mungu kwa tamaa isiyotosheka, lakini hawajawahi kumjua. Walipewa inchi na wamechukua maili, na

wanamfanya “Yesu” kutii kabisa amri zao, na maelekezo yao. Ni nani ambaye ameonyesha huruma kwa huyu Mwana wa Adamu, Ambaye hana mahali pa kuweka kichwa Chake? Ni nani ambaye amewahi kufikiria kushikana mikono Naye kukamilisha agizo la Mungu Baba? Ni nani amewahi kumuwaza? Ni nani mbye amewahi kuyajali matatizo Yake? Bila upendo hata kidogo, mwanadamu anamvuta nyuma na mbele; mwanadamu hajui nuru na uhai wake unatoka wapi na hafanyi chochote isipokuwa kupanga kwa siri jinsi ya kumsulubisha tena “Yesu” wa miaka elfu mbili iliyopita, ambaye amepitia maumivu miongoni mwa wanadamu. Je, “Yesu” anawatia watu moyo kuwa na chuki ya namna hiyo? Je, yote Aliyoyafanya yamesahaulika zamani? Chuki ambayo ilichanganyika kwa maelfu ya miaka itaibuka tena juu. Nyinyi mfano wa Wayahudi! Ni lini “Yesu” amekuwa adui yenu, hadi mmchukie kiasi hicho? Amefanya mengi na kuzungumza mengi—je hakuna chochote chenye manufaa kwenu? Ameyatoa maisha Yake kwenu bila kuomba kurudishiwa kitu chochote, Amejitoa mzima kwenu—kweli bado mnataka kumla Akiwa mzima? Amejitoa kwenu kikamilifu bila kuacha kitu chochote, bila kufurahia utukufu wa kidunia, wema miongoni mwa wanadamu, na upendo miongoni mwa wanadamu, au baraka zote miongoni mwa wanadamu. Watu ni wabinafsi sana Kwake, hajawahi kufurahia utajiri wote wa duniani, Amejitoa kikamilifu, moyo wa upendo wa dhati kwa mwanadamu, Amejirithisha mzima kwa mwanadamu—ni nani ambaye amemfanyia wema? Ni nani aliyewahi kumpatia faraja? Mwanadamu amemjazia mashinikizo yote, balaa yote amempatia Yeye, shida zote mbaya Alizozipitia ni mwanadamu amempatia Yeye, anamtupia lawama kwa uonevu wote, na Amezikubali kimyakimya. Je, Amewahi kumpinga mtu yeyote? Je, Amewahi kuomba fidia hata kidogo kutoka kwa mtu yeyote yule? Ni nani amewahi kumwonyesha huruma yoyote? Kama watu wa kawaida, ni nani miongoni mwenu ambaye hajawahi kuwa na kipindi cha utotoni chenye mapenzi ya dhati? Ni nani ambaye hajawahi kuwa na ujana wa kupendeza? Ni nani ambaye hana joto la wapendwa? Ni nani ambaye hana upendo wa rafiki wa karibu? Ni nani ambaye haheshimiwi na wengine? Ni nani ambaye hana familia yenye upendo? Ni nani ambaye hana faraja ya wandani wao? Je, Amekwishawahi kufurahia moja ya haya? Ni nani ambaye amewahi kumtendea wema hata kidogo? Ni nani ambaye amekwishawahi kumpatia faraja hata kidogo? Ni nani ambaye amekwishawahi kumwonyesha angalau maadili hata kidogo ya kibinadamu? Ni nani ambaye amewahi kuwa mvumilivu Kwake? Ni nani ambaye amewahi kuwa pamoja naye katika nyakati za shida? Ni nani ambaye amewahi kupitia maisha ya shida pamoja Naye? Mwanadamu bado hajaacha kumwomba Yeye; anapeleka tu maombi Kwake bila hata haya, kana kwamba kuja katika ulimwengu wa mwanadamu, Alipaswa kuwa ng’ombe au farasi wake, na Alipaswa kumpatia mwanadamu kila kitu chake; Asipofanya hivyo, mwanadamu hatamsamehe, hatamtendea vizuri, hatamwita Mungu, na hatamheshimu kwa kiwango cha juu. Mwanadamu ni katili sana katika mtazamo wake kwa Mungu, kana kwamba yupo ili kumtesa Mungu hadi kifo, ni baada ya hapo tu ndipo anapunguza maombi yake kwa Mungu; kama sivyo,

mwanadamu hatapunguza kiwango cha matakwa yake kwa Mungu. Inawezekanaje mwanadamu kama huyu asidharauliwe na Mungu? Je, hili si janga la siku hizi? Dhamiri ya mwanadamu haionekani popote. Anasema tu atalipa upendo wa Mungu, lakini anamchanachana Mungu na kumtesa hadi kifo. Je, hii sio “mbinu ya siri” kwa imani yake kwa Mungu, iliyorithishwa kutoka kwa mababu zake? Hakuna mahali ambapo huwezi kuwakuta “Wayahudi,” na leo bado wanafanya kazi ile ile, bado wanafanya kazi ile ile ya kumpinga Mungu, na bado wanaamini kwamba wanamwinua Mungu juu? Inawezekanaje macho ya mwanadamu yamjue Mungu? Inawezekanaje mwanadamu, anayeishi katika mwili, kumchukulia Mungu kama Mungu mwenye mwili ambaye Amekuja kutoka katika Roho? Ni nani miongoni mwa wanadamu anaweza kumjua? Ukweli upo wapi miongoni mwa wanadamu? Haki ya kweli ipo wapi? Ni nani anayeweza kuijua tabia ya Mungu? Ni nani anayeweza kushindana na Mungu mbinguni? Haishangazi kwamba, Alipokuwa miongoni mwa wanadamu, hakuna aliyemjua Mungu, na amekataliwa. Inawezekanaje mwanadamu kuvumilia uwepo wa Mungu? Anawezaje kuvumilia kuruhusu mwanga kuondosha giza la ulimwengu? Je, hii yote si kujitoa kwa heshima kwa mwanadamu? Je, huku sio kuingia adilifu kwa mwanadamu? Je, kazi ya Mungu haijajikita katika kuingia kwa mwanadamu? Ningependa muunganishe kazi ya Mungu na kuingia kwa mwanadamu, na kurekebisha uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu, na kufanya majukumu ambayo yanapaswa kufanywa na mwanadamu kwa uwezo wako wote. Kwa njia hii, kazi ya Mungu hatimaye itafikia mwisho, ikiwa ni pamoja na utukufu Wake!

Tanbihi:

1. “Kuingia kwa mwanadamu” hapa inaonyesha tabia ya mwanadamu ya uasi. Badala ya kutaja kuingia kwa watu katika maisha—ambako ni kuzuri—kunahusu tabia na matendo yao mabaya. Inahusu kwa upana matendo yote ya mwanadamu yaliyo katika upinzani na Mungu.
2. “Wanakerwa na hofu za kubuni” inatumiwa kudhihaki maisha ya binadamu wa mwanadamu yasiyo na mwelekeo. Inahusu hali mbaya ya maisha ya wanadamu, ambayo watu huishi pamoja na pepo.
3. “Bora zaidi” inasemwa kwa dhihaka.
4. “Hamasa yao daima ikiwaka moto zaidi” inasemwa kwa dhihaka, na inahusu hali mbaya ya mwanadamu.
5. “Kumkamata akiwa hai” inahusu tabia ya vurugu na yenye kustahili dharau ya mwanadamu. Mwanadamu ni katili na hayuko tayari kumsamehe Mungu hata kidogo, na hufanya madai ya upuuzi Kwake.
6. “Mpango alioufikiria kwa makini katika akili yake” inasemwa kwa dhihaka, na hii inahusu jinsi watu hawajijui na hawajui kimo chao halisi. Hii ni kauli ya kimatusi.
7. “Wa kuheshimiwa” inasemwa kwa dhihaka.
8. “Kutupa” inaonyesha hali mbaya ya watu ambao hughadhabika kwa hasira wakati ambapo wanashindwa na Mungu. Inaonyesha kiwango cha upinzani wao kwa Mungu.

Maono ya Kazi ya Mungu (1)

Yohana alimfanyia Yesu kazi kwa miaka saba, na tayari alikuwa ameandaa njia Yesu alipofika. Kabla ya haya, injili ya ufalme wa mbinguni iliyohubiriwa na Yohana ilisikika kotekote katika nchi, hivyo ilienea kutoka upande mmoja hadi upande mwingine wa Uyahudi, na kila mtu alimwita nabii. Wakati huo, Mfalme Herode alitamani kumuua Yohana, lakini hakuthubutu, kwani watu walimheshimu sana Yohana, na Herode aliogopa kwamba kama angemuua Yohana wangemuasi. Kazi iliyofanywa na Yohana ilikita mizizi miongoni mwa watu wa kawaida, na aliwafanya Wayahudi kuwa waumini. Kwa miaka saba alimwandalia Yesu njia, mpaka wakati ambapo Yesu alianza kutekeleza huduma Yake. Kwa sababu hii, Yohana alikuwa mkuu zaidi kwa manabii wote. Ilikuwa tu baada ya Yohana kufungwa gerezano ndipo Yesu alianza kazi Yake rasmi. Kabla ya Yohana, hakukuwahi kuwa na nabii aliyemwandalia Mungu njia, kwa sababu kabla ya Yesu, Mungu hakuwa amewahi kupata mwili. Hivyo, kwa manabii wote mpaka Yohana, yeye pekee ndiye angemwandalia Mungu mwenye mwili njia, na kwa jinsi hii Yohana akawa nabii mkuu zaidi wa Agano la Kale na Jipya. Yohana alianza kueneza injili ya ufalme wa mbinguni miaka saba kabla ya ubatizo wa Yesu. Kwa watu, kazi aliyoifanya ilionekana kuwa juu zaidi ya kazi ya baadaye ya Yesu, ilhali yeye alikuwa, hata hivyo, nabii tu. Hakufanya kazi au kuzungumza ndani ya hekalu, lakini katika miji na vijiji nje yake. Hii alifanya, bila shaka, miongoni mwa taifa la Wayahudi, hasa wale waliokuwa maskini. Ni mara chache ambapo Yohana alitangamana na watu kutoka ngazi za juu za jamii, na alieneza injili miongoni mwa watu wa kawaida wa Yudea tu ili kuandaa watu wema kwa Bwana Yesu, na kuandaa maeneo yafaayo Kwake kufanya kazi. Kwa sababu ya kuwa na nabii kama Yohana wa kuandaa njia, Bwana Yesu Alikuwa na uwezo wa kuanzisha njia Yake ya msalaba mara moja punde tu Alipowasili. Wakati Mungu Alipogeuka kuwa mwili ili kufanya kazi yake, hakuwa na jukumu la kufanya kazi ya kuwachagua watu, na hakuwa na haja ya kuwatafuta watu binafsi au mahali ambapo Angefanyia kazi. Hakufanya kazi kama hii Alipokuja; mtu afaaye alikuwa tayari Amemwandalia kabla Yeye hajawasili. Yohana alikuwa tayari amemaliza kazi yake kabla Yesu kuanza kazi Yake, kwani wakati ambapo Mungu mwenye mwili aliwasili kufanya kazi Yake, Alianza kufanya kazi moja kwa moja kwa wale ambao walikuwa wakimngoja kwa muda mrefu. Yesu hakuwa amekuja kufanya kazi ya mwanadamu ya urekebishaji. Alikuwa amekuja tu kutekeleza huduma ambayo ilikuwa Yake kutekeleza, na mengine yote hayakuwa na uhusiano Naye. Yohana alipokuja, hakufanya lolote ila kutoa hekaluni na miongoni mwa Wayahudi kundi la wale waliokubali injili ya ufalme wa mbinguni, ili waweze kuwa vyombo vya kazi ya Bwana Yesu. Yohana alifanya kazi kwa miaka saba, ambapo ni kusema kwamba alieneza injili kwa miaka saba. Wakati wa kazi yake, Yohana hakufanya miujiza mingi, kwa sababu kazi yake ilikua kuandaa njia, ilikuwa kazi ya maandalizi. Kazi zote zingine, kazi ambazo Yesu Alikuwa afanye,

hazikuwa na uhusiano naye; alimwomba mwanadamu tu aungame dhambi zake na atubu, na aliwabatiza watu, ili waweze kuokolewa. Ingawa alifanya kazi mpya, na kufungua njia ambayo kamwe mwanadamu alikuwa bado hajaitembea, bado alimwandalia Yesu njia. Alikuwa nabii tu ambaye alifanya kazi ya maandalizi, na hakuwa na uwezo wa kufanya kazi ya Yesu. Ingawa Yesu hakuwa wa kwanza kuhubiri kuhusu ufalme wa mbinguni, na japokuwa aliendelea na njia ambayo Yohana alianzisha, bado hakukuwa na mwingine ambaye angeweza kufanya kazi yake, na ilikuwa juu zaidi ya kazi ya Yohana. Yesu hangeandaa njia yake mwenyewe; kazi yake ilitekelezwa moja kwa moja kwa niaba ya Mungu. Na hivyo, bila kujali ni miaka mingapi Yohana alifanya kazi, bado alikuwa nabii, na bado yule aliyeandaa njia. Miaka mitatu ya kazi iliyofanywa na Yesu ilizidi miaka saba ya kazi aliyofanya Yohana, kwa kuwa kiini cha kazi yake hakikuwa cha kiwango sawa. Yesu alipoanza kutekeleza huduma Yake, ambao pia ni wakati kazi ya Yohana ilifika mwisho, Yohana alikuwa amewatayarisha watu wa kutosha na mahali pa kutumiwa na Bwana Yesu, na walitosha kwa ajili ya Bwana Yesu kuanza miaka mitatu ya kazi. Na kwa hiyo, punde tu kazi ya Yohana ilipomalizika, Bwana Yesu alianza rasmi kazi Yake Mwenyewe, na maneno yaliyonenwa na Yohana yakarushwa kando. Hiyo ni kwa sababu kazi iliyofanywa na Yohana ilikuwa tu kwa ajili ya mabadiliko, na maneno yake hayakuwa maneno ya uzima ambayo yangemwelekeza mwanadamu kwa ukuaji mpya; mwishowe, maneno yake yalikuwa tu ya matumizi ya muda.

Kazi ambayo Yesu alifanya haikuwa ya mwujiza; kulikuwa na mchakato kwayo, na yote iliendelea mbele kufuatana na sheria za kawaida za vitu. Kufikia miezi sita ya mwisho ya maisha Yake, Yesu alijua kwa uhakika kwamba Alikuwa Amekuja kuifanya kazi hii, na Alijua kwamba Alikuwa Amekuja kupigiliwa misumari msalabani. Kabla ya Yeye kusulubiwa, Yesu alimwomba Mungu Baba siku zote, kama tu Alivyoomba mara tatu katika Bustani la Gethsemane. Baada ya kubatizwa, Yesu alitekeleza huduma Yake kwa miaka mitatu na nusu, na kazi Yake rasmi ilidumu kwa miaka miwili na nusu. Katika mwaka wa kwanza, Alishtakiwa na Shetani, na Akasumbuliwa na mwanadamu, na Akapitia majaribu ya mwanadamu. Alishinda majaribu mengi wakati huo huo Alipotekeleza kazi Yake. Katika miezi sita ya mwisho, wakati ambapo Yesu alikaribia kusulubiwa, kutoka kinywani mwa Petro yalitoka maneno haya kwamba alikuwa Mwana wa Mungu aishiye, kwamba alikuwa Kristo. Ni wakati huo tu ndipo kazi Yake ilijulikana kwa wote, na ni wakati huo tu ndipo utambulisho Wake ulifichuliwa kwa watu wote. Baada ya hilo, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kwamba Angepaswa kusulubiwa kwa ajili ya mwanadamu, na kwamba siku tatu baadaye Angefufuka tena; kwamba Alikuwa Amekuja kutekeleza kazi ya ukombozi, na Yeye alikuwa Mwokozi. Ni katika miezi sita ya mwisho tu ndiyo Alifichua utambulisho Wake na kazi Aliyokusudia kufanya. Huu pia ulikuwa wakati wa Mungu, na kazi ilipaswa kutekelezwa hivyo. Wakati huo, sehemu ya kazi ya Yesu ilikuwa kwa

mujibu wa Agano la Kale, pia na sheria za Musa na maneno ya Bwana wakati wa kipindi cha Enzi ya Sheria. Yote hayo Yesu Alitumia kufanya sehemu ya kazi yake. Alihubiri kwa watu na kuwafundisha kwenye masinagogi, na yeye Alitumia utabiri wa manabii katika Agano la Kale kuwakemea Mafarisayo waliokuwa na uhasama Naye, na Alitumia maneno katika Maandiko kufichua uasi wao na hivyo kuwahukumu. Kwa maana wao walidharau mambo ambayo Yesu Aliyafanya; hasa, nyingi ya kazi ya Yesu haikufuatana na sheria katika Maandiko, na zaidi ya hayo, kile Alichofundisha kilikuwa kikuu kuliko maneno yao wenyewe, na hata kikubwa kuliko kile ambacho kilikuwa kimetabiriwa na manabii katika Maandiko. Kazi ya Yesu ilikuwa kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu na kusulubiwa tu. Kwa hivyo, hakukuwa na haja Kwake kusema maneno zaidi ili kumshinda mtu yeyote. Mengi ya yale Aliyomfundisha mwanadamu yalitolewa kutoka kwa Maandiko, na hata kama kazi yake haikuzidi Maandiko, bado Aliweza kutimiza kazi ya kusulubiwa. Yake haikuwa kazi ya neno, wala kwa ajili ya kumshinda mwanadamu, lakini kwa minajili ya kumkomboa mwanadamu. Yeye Alihusika kama dhabihu ya dhambi tu kwa mwanadamu, na hakuhusika kama chanzo cha Neno kwa mwanadamu. Hakufanya kazi ya watu wa Mataifa mengine, ambayo ilikuwa kazi ya kumshinda mwanadamu, bali Alifanya kazi ya kusulubiwa, kazi ambayo ilifanywa miongoni mwa wale ambao waliamini kulikuwa na Mungu. Japokuwa kazi yake ilifanywa juu ya msingi wa Maandiko, na Alitumia yale yaliyotabiriwa na manabii wa kale kuwahukumu Mafarisayo, hii ilikuwa ya kutosha kukamilisha kazi ya kusulubiwa. Kama kazi ya leo ingekuwa bado inafanyika juu ya misingi ya utabiri wa manabii wa kale katika Maandiko, basi haingewezekana nyinyi kushindwa, kwa kuwa Agano la Kale halina kumbukumbu ya uasi na dhambi zenu nyinyi watu wa China, hakuna historia ya dhambi zenu. Kwa hivyo, kama kazi hii bado ingedumu katika Biblia, hamngeweza kutoa matunda. Biblia inaandika lakini kwa uchache historia ya wana wa Israeli, ambayo haina uwezo wa kusadikisha iwapo nyinyi ni waovu ama wema, ama ya kukuhukumu. Hebu Fikiria kama Ngingekuwa wa kuwahukumu nyinyi kadri ya historia ya wana wa Israeli—bado mngenifuata Mimi kama mnavyonifuata hivi leo? Je, mnajua jinsi ambavyo nyinyi m wagumu? Kama hakuna maneno ambayo yalisemwa wakati wa awamu hii, basi itakuwa vigumu kukamilisha kazi ya ushindi. Kwa sababu Mimi sijakuja kugongomewa msumari msalabani, sharti Mimi niseme maneno ambayo ni tofauti na yatokayo kwa Biblia, ilimradi muweze kushindwa. Kazi iliyofanywa na Yesu ilikuwa tu hatua moja juu zaidi ya Agano la Kale; ilitumiwa kuianza enzi, na kuiongoza enzi hiyo. Kwa nini Alisema, “Sikuja kuharibu sheria, bali kuitimiza”? Lakini katika kazi Yake kulikuwa na mengi ambayo yalitofautiana na sheria zilizotumika na amri zilizofuatwa na Waisraeli wa Agano la Kale, kwani Hakuja kuitii sheria, bali kuitimiza. Mchakato wa kuitimiza ulikuwa pamoja na mambo mengi halisi: Kazi Yake ilikuwa ya vitendo zaidi na halisi, na, aidha, ilikuwa hai, na hakukuwa tu kufuata masharti bila kufikiri. Je, Waisraeli hawakuitii Sabato? Yesu alipokuja Hakuitii Sabato, kwani Alisema

kwamba Mwana wa Adamu alikuwa Bwana wa Sabato, na wakati ambapo Bwana wa Sabato alikuja, Angefanya Alivyopenda. Alikuwa Amekuja kutimiza sheria za Agano la Kale na kuzibadilisha sheria. Yote ambayo hufanywa leo ni kwa msingi wa siku hizi, lakini bado yako juu ya msingi wa kazi ya Bwana katika Enzi ya Sheria, na hayavuki mipaka ya eneo hili. Kuulinda ndimi zenu, na kutozini, kwa mfano—Je, hizi si sheria za Agano la Kale? Leo, kile kinachotakikana kwenu sio chenye upeo wa amri kumi tu, lakini ni kuwa na amri na sheria ambazo zina ukuu kuliko hizo zilizokuja hapo awali, ila hii haina maana kuwa kile kilichokuja hapo awali kimeondolewa, kwa kuwa kila awamu ya kazi ya Mungu hufanywa juu ya msingi wa awamu ambayo ilikuja hapo awali. Na kuhusu kile ambacho Yehova aliwasilisha kwa Israeli, kama vile kuwahitaji watu kutoa sadaka, kuwaheshimu wazazi wao, kutoabudu sanamu, kutowadhulumu au kutukana wengine, kutozini, kutovuta sigara au kutokunywa pombe, na kutokula nyamafu au kunywa damu, je, huo si muundo msingi wa utendaji wenu hata leo? Kazi iliyotekelezwa hadi leo iko juu ya msingi wa mambo ya zamani. Ingawa sheria za zamani hazitajwi tena, nawe umewekewa madai mapya, sheria hizi mbali na kufutwa, badala yake, zimeinuliwa katika hadhi ya juu zaidi. Kusema kwamba zimefutwa kuna maana kwamba enzi ya awali imepitwa na wakati, wakati kuna amri zingine ambazo lazima uzitii milele yote. Amri za zamani tayari zimetwa katika vitendo, tayari zimekuwa nafsi ya mwanadamu, na hakuna haja ya kurudia kusema amri za kutovuta sigara, kutokunywa pombe, na kadhalika. Juu ya msingi huu, amri mpya zimeagizwa kufuatana na mahitaji yenu leo, kufuatana na kimo chenu, na kufuatana na kazi ya leo. Kutangaza amri kwa ajili ya enzi mpya hakumaanishi kufuta amri za enzi ya kale, bali kuziinua juu zaidi ya msingi huu, kuyafanya matendo ya mwanadamu kuwa kamili zaidi, na kufuatana na uhalisi zaidi. Kama, leo, mngetaikiwa tu kufuata amri na kutii sheria za Agano la Kale, kwa namna sawa na wana wa Israeli, na kama, hata, nyinyi mlitakiwa mkariri sheria ambazo ziliwekwa na Bwana, hakungekuwa na uwezekano kwamba mngeweza kubadilika. Kama mngekuwa tu mnatakiwa kutii zile amri chache zilizo na mipaka ama kukariri sheria zisizohesabika, asili zenu za zamani zingebaki zimekita mizizi, na hakungekuwa na mbinu ya kuzing'oa. Hivyo mngeendelea kuzidi kupotoshwa, na hakuna hata mmoja wenu angeweza kuwa mtiifu. Ambayo ni kusema kwamba amri chache rahisi au sheria zisizohesabika hazina uwezo wa kuwasaidia kujua matendo ya Yehova. Nyinyi si sawa na wana wa Israeli: kwa kufuata sheria na kukariri amri waliweza kushuhudia matendo ya Yehova, na kumpa Yeye pekee ibada yao, lakini hamwezi kufanikisha hili, na amri chache za Agano la Kale haziwezi tu kuwafanya nyinyi kupeana mioyo yenu, au kuwalinda, lakini badala yake itawafanya muwe wazembe, na kuwateremsha mpaka Kuzimu. Kwa sababu kazi Yangu ni kazi ya ushindi, na inalenga uasi wenu na asili yenu ya zamani. Maneno yenye huruma ya Yehova na Yesu yanapungukiwa mno na maneno makali ya hukumu leo. Bila maneno makali kama haya, ingekuwa vigumu kuwashinda ninyi “wataalam,” ambao mmekua wasiotii kwa miaka elfu nyingi. Sheria za Agano

la Kale zilipoteza nguvu zake kwenu kwa muda mrefu uliopita, na hukumu ya leo ni ya kuogofya mno kuliko sheria za zamani. Ya kuwafaa nyinyi zaidi ni hukumu, na wala si vikwazo duni vya sheria, kwa kuwa ninyi si wanadamu wa mwanzo kabisa, lakini wanadamu ambao wamekuwa fisadi kwa miaka elfu nyingi. Kile ambacho mwanadamu lazima atimize sasa ni kulingana na hali halisi ya mwanadamu leo, kulingana na tabia bora na kimo halisi cha mwanadamu wa siku hizi, na hakihitaji kwamba wewe ufuate mafundisho ya dini. Hii ni kwa minajili ya mabadiliko yaweze kupatikana katika asili zako za zamani, na ili uweze kutupa kando dhana zako. Je, unadhani sheria hizi ni mafundisho ya dini? Hizo ni, inaweza kusemwa, masharti ya kawaida kwa mwanadamu. Hayo si mafundisho ya dini unayotakiwa kufuata. Chukua mfano wa, kukataza kuvuta sigara—je, hayo ni mafundisho ya dini? Hayo si mafundisho ya dini! Yanahitajika na ubinadamu wa kawaida; si mafundisho ya dini, bali ni sheria kwa wanadamu wote. Leo, idadi kubwa au zaidi ya amri ambazo zimetangazwa si sheria; ni kinachohitajika ili kutimiza ubinadamu wa kawaida. Watu hawakuwa na au kujua vitu kama hivyo zamani, na kwa hiyo wanatakiwa kuvitimizea leo, ambavyo havihesabiki kama mafundisho ya dini. Sheria si sawa na mafundisho ya dini. Mafundisho ya dini Ninayozungumzia yanahusu sherehe, urasmi au desturi za mwanadamu za kuacha maadili na zenye kosa; ni masharti na kanuni ambazo hazimsaidii mwanadamu, hazina manufaa kwake, na ni kusudi la kitendo lisilo na umuhimu. Hiki ni kifano cha mafundisho ya dini, na mafundisho ya dini kama hayo lazima yaachwe, kwani hayampi mwanadamu manufaa yoyote. Ni yale yaliyo ya manufaa kwa mwanadamu ndiyo yanatakiwa kutiwa katika vitendo.

Maono ya Kazi ya Mungu (2)

Enzi ya Neema ilihubiri injili ya toba, na alimradi mwanadamu aliamini, basi angeokolewa. Leo, badala ya wokovu kuna majadiliano tu ya ushindi na ukamilifu. Haisemwi katu kwamba mtu mmoja akiamini, familia yake yote itabarikiwa, au kwamba wokovu ni ya mara moja na kwa wote. Leo, hakuna mtu anayezungumza maneno haya, na vitu kama vile vimepitwa na wakati. Wakati huo kazi ya Yesu ilikuwa ni ukombozi wa wanadamu wote. Dhambi za wote ambao walimwamini zilisamehewa; ilimradi wewe ulimwamini, Angeweza kukukomboa wewe; kama wewe ulimwamini Yeye, wewe hukuwa tena mwenye dhambi, wewe ulikuwa umeondolewa dhambi zako. Hii ndiyo ilikuwa maana ya kuokolewa, na kuhesabiwa haki kwa imani. Hata hivyo, kati ya wale walioamini, kulibaki na kitu ambacho kilikuwa na uasi na pingamizi kwa Mungu, na ambacho kilibidi kiondolewe polepole. Wokovu haukuwa na maana kuwa mwanadamu alikuwa amepatwa na Yesu kabisa, lakini ni kuwa mwanadamu hakuwa tena mwenye dhambi, na kuwa alikuwa amesamehewa dhambi zake; mradi tu uliamini, wewe kamwe hungekuwa mwenye dhambi. Wakati huo, Yesu alifanya kazi kubwa ambayo haikueleweka kwa wanafunzi Wake, na kusema mengi kwamba watu hawakuelewa. Hii ni kwa sababu, wakati huo,

Hakutoa maelezo. Kwa hivyo, miaka kadhaa baada ya Yeye kuondoka, Mathayo aliunda kizazi chake, na wengine pia walifanya kazi kubwa ambayo ilikuwa ya mapenzi ya mwanadamu. Yesu hakuja kumkamilisha na kumpata mwanadamu, lakini kufanya awamu moja ya kazi: kuleta injili ya ufalme wa mbinguni na kukamilisha kazi ya kusulubiwa—na punde tu Yesu Aliposulubishwa, kazi Yake ilifika mwisho kamili. Lakini kwa awamu iliyoko sasa—kazi ya ushindi—maneno mengi zaidi lazima yasemwe, kazi nyingi zaidi lazima ifanywe, na lazima kuwe na hatua nyingi. Hivyo pia ni lazima siri za kazi ya Yesu na Yehova zitafichuliwa, ili wanadamu wote waweze kuwa na ufahamu na uwazi wa imani yao, kwa kuwa hii ni kazi ya siku za mwisho, na siku za mwisho ni mwisho wa kazi ya Mungu, wakati wa kuhitimisha kazi hii. Hii awamu ya kazi itakufafanulia sheria ya Yehova na ukombozi wa Yesu, na ni hasa ili uweze kuelewa kazi nzima ya mpango wa usimamizi wa Mungu wa miaka elfu sita, na kuelewa umuhimu na kiini cha mpango huu wa usimamizi wa miaka elfu sita, na kuelewa kusudi la kazi zote Alizozifanya Yesu na maneno Aliyoyasema, na hata upofu wako wa imani kwenye na katika ibada ya Biblia. Yote haya yatakuwezesha kuelewa kabisa. Wewe utakuja kufahamu kazi anayoifanya Yesu na kazi ya Mungu leo; utaelewa na kushuhudia ukweli wote, uzima, na njia. Katika awamu ya kazi Aliyoifanya Yesu, kwa nini Yesu Aliondoka bila kufanya kazi ya ukamilishaji? Kwa sababu awamu ya kazi ya Yesu haikuwa kazi ya kukamilisha. Wakati Yeye Alisulubishwa msalabani, maneno Yake pia yalifika mwisho; baada ya kusulubiwa kwake, kazi Yake kwa hivyo ilimalizika. Awamu ya sasa ni tofauti. Ni baada tu ya maneno hayo kusemwa hadi mwisho na kazi nzima ya Mungu iwe imehitimika ndipo kazi yake itakapokuwa imemalizika. Wakati wa awamu ya kazi ya Yesu, kulikuwa na maneno mengi yaliyobakia bila kusemwa, au ambayo hayakuwa yameelezwa kikamilifu kwa ufasaha. Waama, Yesu hakujali Alichosema au kile ambacho hakusema, kwa kuwa huduma yake haikuwa huduma ya maneno; na hivyo baada ya Yeye kusulubishwa msalabani Aliondoka. Awamu hiyo ilikuwa hasa kwa ajili ya kusulubiwa, na ni tofauti na awamu ya sasa. Awamu ya kazi hii ni hasa kwa ajili ya kukamilisha, kufumbua, na kuleta kazi yote kwenye hitimisho. Kama maneno hayasemwi hadi tamati yake kabisa, hakutakuwa na mbinu ya kuhitimisha kazi hii, kwa kuwa awamu hii ya kazi yote inafikishwa mwisho na kukamilika kwa kutumia maneno. Wakati huo, Yesu Alifanya kazi kubwa isiyoeleweka na mwanadamu. Akaondoka kimyakimya, na leo bado kunao wengi wasioelewa maneno Yake, ambao ufahamu wao ni potofu lakini bado unaaminika nao kwamba ni sahihi, ambao hawajui kuwa wao si sahihi. Mwishoni, awamu hii ya sasa itafikisha kazi ya Mungu mwisho ulio kamilifu, na kutoa hitimisho Lake. Wote watakuja kufahamu na kujua mpango wa usimamizi wa Mungu. Dhana zilizo ndani ya mwanadamu, nia yake, fahamu yake potofu, dhana zake kuhusu kazi ya Yehova na Yesu, maoni yake kuhusu watu wa Mataifa mengine na michepuko yake ingine na makosa yake yatarekebishwa. Na mwanadamu ataelewa njia yote ya haki ya uzima, na kazi yote anayofanya Mungu, na ukweli wote. Wakati hayo

yatafanyika, awamu hii ya kazi itafikia kikomo. Kazi ya Yehova ilikuwa uumbaji wa ulimwengu, ilikuwa mwanzo; awamu hii ya kazi ni mwisho wa kazi, na ni hitimisho. Hapo mwanzo, kazi ya Mungu ilifanyika miongoni mwa wateule wa Israeli, na ilikuwa mapambazuko ya kipindi kipya katika pahali patakatifu zaidi ya popote. Awamu ya mwisho ya kazi inafanywa katika nchi ambayo ni chafu zaidi ya zote, kuhukumu ulimwengu na kuleta enzi kwenye kikomo. Katika awamu ya kwanza kazi ya Mungu ilifanyika katika maeneo yenye kung'aa kuliko maeneo yote, na awamu ya mwisho inafanyika katika maeneo yaliyo katika giza kuliko maeneo yote, na giza hili litaondolewa, na mwanga kufunguliwa, na watu wote kushindwa. Wakati watu wa maeneo haya yaliyo chafu kuliko yote na yaliyo na giza watakuwa wameshindwa na idadi yote ya watu wametambua kuwa Mungu yupo, na ya kuwa ni Mungu wa kweli, na kila mtu Amemwamini kabisa, basi ukweli huu utatumika kutekeleza kazi ya ushindi katika ulimwengu mzima. Awamu hii ya kazi ni ya ishara: Punde tu kazi ya kipindi hiki itakapomalizika, kazi ya miaka 6,000 ya usimamizi itafikia mwisho kabisa. Mara baada ya wale walioko katika maeneo yaliyo na giza kuliko yote watakapokuwa wameshindwa, bila shaka itakuwa hivyo pia kila mahali pengine. Kwa hivyo, kazi ya ushindi tu katika China inabeba ishara ya maana. China inajumuisha nguvu zote za giza, na watu wa China wanawakilisha wale wote ambao ni wa mwili, wa Shetani, na wa mwili na damu. Ni watu wa China ndio wamepotoshwa sana na joka kubwa jekundu, ambao wana upinzani wenye nguvu dhidi ya Mungu, ambao wana ubinadamu ulio mbovu zaidi na ulio mchafu, na kwa hivyo hao ni umbo asili la wanadamu wote wenye matendo maovu. Hii si kusema kwamba nchi nyingine hazina shida kabisa; dhana za mwanadamu ni sawa zote, na ingawa watu wa nchi hizi wanaweza kuwa na uhodari mzuri, ikiwa hawamjui Mungu, basi ni lazima iwe kwamba wanampinga. Kwa nini Wayahudi pia walimpinga na kumwasi Mungu? Kwa nini Mafarisayo pia walimpinga? Kwa nini Yuda alimsaliti Yesu? Wakati huo, wengi wa wanafunzi hawakumjua Yesu. Kwa nini, baada ya Yesu kusulubiwa na kufufuliwa tena, watu bado hawakumwamini? Je, uasi wa mwanadamu sio sawa wote? Ni tu kwamba watu wa China wamefanyika mfano, na watakaposhindwa watakuwa mfano na kielelezo, na watatumika kama kumbukumbu kwa wengine. Kwa nini mimi daima Nimesema yakuwa nyinyi ni kiungo cha mpango wangu wa usimamizi? Ni katika watu wa China ambapo upotovu, uchafu, udhalimu, upinzani, na uasi unadhihirishwa kikamilifu zaidi na kufichuliwa kwa hali zao mbalimbali. Kwa upande mmoja, wao ni wa kimo cha umaskini, na kwa upande mwingine, maisha yao na mawazo yao ni ya nyuma kimaendeleo, na tabia zao, mazingira ya kijamii, familia ya kuzaliwa—yote ni ya umaskini na ya nyuma kimaendeleo kuliko yote. Hadhi yao, pia, ni ya chini. Kazi katika eneo hili ni ya ishara, na baada ya kazi hii ya majaribio hufanywa kwa ukamilifu wake, na kazi yake inayofuata itakwenda vizuri zaidi. Kama awamu hii ya kazi inaweza kukamilika, basi kazi inayofuata itakamilika bila shaka. Mara baada ya awamu ya kazi hii kutimizwa, na mafanikio makubwa kufikiwa kikamilifu, kazi ya ushindi katika ulimwengu mzima itakua imefikia kikomo

kamili. Kwa kweli, mara baada ya kazi miongoni mwenu imekuwa ya mafanikio, hii itakuwa sawa na mafanikio katika ulimwengu mzima. Huu ndio umuhimu wa sababu Yangu kuwafanya mfano wa kuigwa na kielelezo. Uasi, upinzani, uchafu, udhalimu—yote haya hupatikana kwa watu hawa, na ndani yao pamewakilishwa uasi wote wa wanadamu. Wao ni wa kushangaza kweli. Hivyo, wanafanywa kuwa mfano wa ushindi, na punde tu watakaposhindwa watakuwa kama ilivyo kawaida kielelezo na mfano wa kuigwa na wengine. Hakuna kilichokuwa cha ishara zaidi ya awamu ya kwanza iliyofanyika katika Israeli: Waisraeli walikuwa watakatifu sana na wenye upotovu wa chini zaidi kuliko watu wote, na hivyo pambazuko la kipindi kipya katika nchi hii kilibeba umuhimu mkubwa. Inaweza kusemwa kwamba mababu wa wanadamu walitoka Israeli, na kwamba Israeli, ilikuwa watani wa kazi ya Mungu. Hapo mwanzo, watu hawa walikuwa watakatifu sana, na wote walimwabudu Yehova, na kazi ya Mungu ndani yao iliweza kuzaa mazao makubwa. Biblia nzima inarekodi kazi ya enzi mbili: Moja ilikuwa kazi ya Enzi ya Sheria, na moja ilikuwa kazi ya Enzi ya Neema. Agano la Kale hurekodi maneno ya Yehova kwa Waisraeli na kazi Yake katika Israeli; Agano Jipya linarekodi kazi ya Yesu huko Uyahudi. Lakini kwa nini Biblia haina majina yoyote ya Kichina? Kwa sababu sehemu mbili za kwanza za kazi ya Mungu zilifanyika katika Israeli, kwa sababu watu wa Israeli walikuwa wateule—ambayo ni kusema kwamba wao walikuwa wa kwanza kukubali kazi ya Bwana. Walikuwa wenye upotovu wa chini zaidi ya wanadamu wote, na hapo mwanzo, walikuwa na nia ya kumtazamia Mungu na kumheshimu Yeye. Walitii maneno ya Bwana, na daima walitumika katika hekalu, na walivaa mavazi ya kikuhani au mataji. Walikuwa watu wa kwanza kabisa kuabudu Mungu, na chombo cha kwanza kabisa cha kazi yake. Watu hawa walikuwa kielelezo na mfano wa kuiga kwa wanadamu wote. Walikuwa kielelezo na mfano wa kuiga wa utakatifu na haki. Watu kama Ayubu, Ibrahim, Lutu, au Petro na Timotheo—wote walikuwa Waisraeli, na vielelezo na mifano mitakatifu zaidi ya watu wote. Israeli ilikuwa nchi ya kwanza ya kuabudu Mungu miongoni mwa wanadamu wote, na watu wengi wenye haki walitoka hapa kuliko mahali pengine popote. Mungu Alifanya kazi kati yao ili aweze kusimamia vizuri mwanadamu katika nchi zote na katika siku zijazo. Mafanikio yao na haki ya ibada yao ya Yehova yaliandikwa kwenye kumbukumbu, ili waweze kuhudumu kama vielelezo na mifano kwa watu waliokuwa nje ya Israeli wakati wa Enzi ya Neema; na matendo yao yamezingatia miaka elfu kadhaa ya kazi, mpaka hivi leo.

Baada ya kuanzishwa kwa dunia, hatua ya kwanza ya kazi ya Mungu ilifanyika katika Israeli, na hivyo Israeli palikuwa mahali pa kuzaliwa kwa kazi ya Mungu duniani, na msingi wa kazi ya Mungu duniani. Upeo wa kazi ya Yesu ulienea kote Uyahudi. Wakati wa kazi Yake, wachache sana wa wale waliokuwa nje ya Uyahudi walijua jambo hilo, kwa kuwa hakufanya kazi yoyote nje ya Uyahudi. Leo, kazi ya Mungu imeletwa nchini China, na inatekelezwa kabisa

ndani ya eneo hili. Katika awamu hii, hakuna kazi inayozinduliwa nje ya China; kuenea kwake zaidi ya China ni kazi ambayo itakuja baadaye. Hatua hii ya kazi inafuatilia kutoka kwa hatua ya kazi ya Yesu. Yesu alifanya kazi ya ukombozi, na hatua hii ni kazi inayofuata; ukombozi umekamilika, na katika hatua hii hakuna haja ya kuzaliwa na Roho Mtakatifu, kwa sababu hatua hii ya kazi ni tofauti na hatua ya mwisho, na, zaidi ya hayo, kwa sababu China ni tofauti na Israeli. Hatua ya kazi iliyofanywa na Yesu ilikuwa kazi ya ukombozi. Mtu alimwona Yesu, na si muda mrefu baadaye, kazi Yake ilianza kuenea kwa Wayahudi. Leo, kuna wengi ambao wanaamini katika Mungu katika Amerika, Uingereza na Urusi, hivyo kwa nini kuna wachache nchini China? Kwa sababu China ni taifa lililotengwa zaidi. Kwa hivyo, China ilikuwa ya mwisho kukubali njia ya Mungu, na hata sasa imekuwa chini ya miaka mia tangu kuikubali—baadaye zaidi ya Amerika na Uingereza. Hatua ya mwisho ya kazi ya Mungu inafanywa katika nchi ya China ili kutamatisha kazi Yake, na ili kazi Yake yote iweze kukamilika. Watu wa Israeli wote walimwita Yehova, Bwana wao. Wakati huo, walimwona kama kichwa cha familia zao, na Israeli yote ikawa familia kubwa ambapo kila mtu alimwabudu Bwana wao Yehova. Roho wa Bwana mara nyingi Aliwatokea, naye akanena na kutamka sauti Yake, na kutumia nguzo ya wingu na sauti kuongoza maisha yao. Wakati huo, Roho alitoa mwongozo Wake katika Israeli moja kwa moja, Akizungumza na kutoa sauti Yake kwa watu, na waliona mawingu na kusikia sauti za ngurumo, na kwa njia hii Aliyaongoza maisha yao kwa maelfu kadhaa ya miaka. Kwa hiyo, watu wa Israeli pekee wamekuwa wakimwabudu Yehova daima. Wanaamini kwamba Yehova ni Mungu wao, na si Mungu wa Mataifa. Hii haishangazi: Yehova, hata hivyo, alikuwa amefanya kazi kati yao kwa karibu miaka 4,000. Katika nchi ya China, baada ya maelfu ya miaka ya kulala kwa uchovu, sasa tu ndipo wapotovu wamejua kwamba mbingu na ardhi na vitu vyote hazikuundwa kwa kawaida, bali zilifanywa na Muumba. Kwa sababu injili hii imekuja kutoka nje ya nchi, hao wenye mawazo ya kikabaila, wapinga mageuzi wanaamini kwamba wote wanaokubali injili hii wanafanya uhalifu mkubwa, ni vijibwa wanaomsaliti Budha—babu wao. Zaidi ya hayo, wengi wa wenye mawazo haya ya kikabaila wanauliza, Watu wa China wanawezaje kuamini katika Mungu wa wageni? Je, hawawasaliti baba zao? Je, hawatendi mabaya? Leo, watu wamesahau kitambo kwamba Yehova ndiye Mungu wao. Wamemsukuma Muumba nyuma ya akili zao kitambo, na badala yake wanaamini katika nadharia ya mageuko, ambayo ina maana kwamba mtu amebadilika kutoka kuwa sokwe, na kwamba ulimwengu wa asili ulikuja kama jambo la lazima. Chakula chochote kizuri kinachofurahiwa na wanadamu kinatolewa na ulimwengu, kuna utaratibu wa maisha na kifo cha mwanadamu, na hakuna Mungu anayetawala vyote. Zaidi ya hayo, kuna watu wengi wasioamini Mungu ambao wanaamini kwamba Mungu kutawala kila kitu ni ushirikina na si jambo la kisayansi. Lakini je, sayansi inaweza kuchukua nafasi ya kazi ya Mungu? Je, sayansi inaweza kutawala juu ya wanadamu? Kuhubiri injili katika nchi ambayo inatawaliwa na kutomwamini Mungu siyo kazi rahisi, na

inahusisha vikwazo vingi. Leo, je, si kuna wengi ambao wanapinga Mungu kwa njia hii?

Yesu alipokuja kufanya kazi Yake, watu wengi walilinganisha kazi Yake dhidi ya kazi ya Yehova, walipopata kwamba hazilingani, walimsulubisha Yesu msalabani. Kwa nini hawakupata mambo yanayofanana katika kazi Zao? Ilikuwa, kwa sehemu, kwa sababu Yesu alifanya kazi mpya, na pia kwa sababu kabla ya Yesu kuanza kazi Yake, hakuna mtu aliyeandika ukoo Wake. Kama mtu angefanya hivyo, basi kusingekuwa na haja ya kuwa na wasiwasi, na nani bado angempigilia misumari Yesu msalabani? Ikiwa Mathayo angeandika ukoo wa Yesu miongo kadhaa kabla, basi Yesu asingepitia mateso hayo makuu. Je, si hivyo? Mara tu watu walipojifunza kuhusu uzao wa Yesu—kwamba alikuwa mwana wa Ibrahimu, na mzao wa Daudi—basi wangekoma kumtesa Yeye. Je, si jambo la kusikitisha kwamba uzazi Wake ulikawia mno kuandikwa? Na ni jambo la kusikitisha kwamba Biblia inarekodi tu hatua mbili za kazi ya Mungu: hatua moja ambayo ilikuwa kazi ya Enzi ya Sheria, na moja ambayo ilikuwa kazi ya Enzi ya Neema; hatua moja ambayo ilikuwa kazi ya Bwana, na moja ambayo ilikuwa kazi ya Yesu. Ingekuwa bora zaidi kama nabii mkuu angetabiri kazi ya leo. Kungekuwa na sehemu ya ziada ya Biblia yenye mada “Kazi ya Siku za Mwisho”—je, si hiyo ingekuwa bora sana? Kwa nini mtu lazima apitie ugumu sana leo? Mlikuwa na wakati mgumu sana! Ikiwa mtu yeyote anastahili kuchukiwa, ni Isaya na Danieli kwa ajili ya kutotabiri kazi ya siku za mwisho, na kama mtu yeyote anastahili kulaumiwa, ni mitume wa Agano Jipya ambao hawakuandika orodha ya uzazi wa kupata mwili kwa Mungu kwa mara ya pili mapema. Aibu iliyoje! Mnalazimika kutafuta ushahidi kila mahali, na hata baada ya kupata vipande kiasi vya maneno madogo bado hamwezi kujua kama kweli ni ushahidi. Aibu iliyoje! Kwa nini Mungu ni msiri sana katika kazi Yake? Leo, watu wengi bado hawajapata ushahidi thabiti, lakini pia hawawezi kukataa. Basi wanapaswa kufanya nini? Hawawezi kumfuata Mungu kwa uthabiti, wala pia hawawezi kuendelea mbele katika shaka hiyo. Na hivyo, “wasomi mahiri na wenye vipawa” wengi hukubali mtazamo wa “jaribu na kuona” wanapomfuata Mungu. Hii ni shida nyingi sana! Je, si mambo yangekuwa rahisi sana kama Mathayo, Mariko, Luka na Yohana wangeweza kutabiri yajayo? Ingekuwa bora kama Yohana angekuwa ameona ukweli wa ndani wa uzima katika ufalme—ni jambo la kusikitisha sana kwamba yeye aliona tu maono na hakuona kazi halisi, yakinifu duniani. Aibu iliyoje! Ni nini kibaya na Mungu? Kwa nini, baada ya kazi yake kwenda vizuri sana katika Israeli, sasa Amefika China, na kwa nini alipaswa kuwa mwili, na kufanya kazi na kuishi kati ya watu? Mungu hamfikirii mtu kabisa! Sio tu kwamba Hakuwaambia watu mapema, lakini pia ghafla Alileta adabu na hukumu Yake. Kwa kweli haileti maana! Mara ya kwanza Mungu kuwa mwili, Aliteseka dhiki nyingi kutokana na kutomwambia mwanadamu ukweli wote wa ndani mapema. Hakika Yeye Hawezi kuwa Amesahau hilo? Na kwa nini bado Hamwambii mtu wakati huu? Leo, ni bahati mbaya kwamba kuna vitabu sitini na

sita tu katika Biblia. Kunahitaji tu kuwa na mmoja zaidi unaotabiri kazi ya siku za mwisho! Je, hufikiri? Hata Yehova, Isaya na Daudi hawakutaja kazi ya leo. Waliondolewa zaidi kutoka wakati wa sasa, na utengano wa muda wa zaidi ya miaka 4,000. Wala Yesu hakubashiri kikamilifu kazi ya leo, Akizungumzia kidogo tu, na bado mtu hupata ushahidi mchache. Ukilinganisha kazi ya leo na ya awali, zote mbili zinawezaje kulingana? Hatua ya kazi ya Yehova ilielekezwa kwa Israeli, hivyo ukilinganisha kazi ya leo nayo kutakuwa na hitilafu kubwa hata zaidi; hizo mbili haziwezi kulinganishwa kabisa. Wala wewe si wa Israeli, au Myahudi; uhodari wako na kila kitu kinachokuhusu kina upungufu—unawezaje kujilinganisha nao? Je, hii inawezekana? Jua kwamba leo ni Enzi ya Ufalme, na ni tofauti na Enzi ya Sheria na Enzi ya Neema. Kwa hali yoyote, usijaribu kutumia fomyula; Mungu hawezi kupatikana katika fomyula yoyote kama hiyo.

Yesu aliishije katika kipindi cha miaka 29 baada ya kuzaliwa Kwake? Biblia haina kumbukumbu yoyote ya utoto na ujana Wake; unajua yalivyokuwa? Inawezekana kuwa hakuwa na utoto au ujana, na kwamba alipozaliwa alikuwa tayari mwenye umri wa miaka 30? Unajua kidogo sana, hivyo usiwe mzembe unapotoa maoni yako. Haikupi faida! Biblia inarekodi tu kwamba kabla ya siku ya kuzaliwa ya 30, Yesu alibatizwa na Aliongozwa na Roho Mtakatifu kwenda jangwani kupitia jaribio la shetani. Na Injili Nne inarekodi kazi Yake ya miaka kumi na tatu na nusu. Hakuna rekodi ya utoto na ujana Wake, lakini hii haithibitishi kuwa Hakuwa na utoto na ujana; ni kwamba tu, mwanzoni, Hakufanya kazi yoyote, na Alikuwa mtu wa kawaida. Kwa hivyo, unaweza kusema kwamba Yesu aliishi kwa miaka 33 bila ujana au utoto? Inawezekana kwamba Alifika umri wa miaka 33 na nusu ghafla? Kila ambacho mtu huyu anafikiria kumhusu Yeye ni cha miujiza na kisichowezekana. Hakuna shaka kwamba Mungu mwenye mwili ana ubinadamu wa kawaida na wa desturi, lakini Anapotekeleza kazi Yake ni moja kwa moja na ubinadamu Wake usio kamili na uungu Wake kamili. Ni kwa sababu ya hili watu wana mashaka juu ya kazi ya leo, na hata juu ya kazi ya Yesu. Ingawa kazi ya Mungu inatofautiana katika mara mbili Anapokuwa mwili, dutu Yake haitofautiani. Bila shaka, ukisoma kumbukumbu za Injili Nne, tofauti ni kuu. Unawezaje kurudi kwenye maisha ya Yesu wakati wa utoto na ujana Wake? Unawezaje kuelewa ubinadamu wa kawaida wa Yesu? Labda una ufahamu thabiti wa ubinadamu wa Mungu leo, lakini hufahamu ubinadamu wa Yesu, hata zaidi hauuelewi. Ingingeandikwa na Mathayo, usingekuwa na fununu ya ubinadamu wa Yesu. Labda, Nitakapokuambia kuhusu hadithi za Yesu wakati wa maisha Yake, na kukuambia ukweli wa ndani wa utoto na ujana wa Yesu, utatikisa kichwa chako: Hapana! Haiwezekani kuwa Alikuwa hivyo. Hawezi kuwa na udhaifu wowote, sembuse kuwa na ubinadamu wowote! Hata utapaza sauti na kupiga yowe. Ni kwa sababu humjui Yesu kwamba una dhana juu Yangu. Unamwamini Yesu kuwa mwenye uungu pia, kuwa bila kitu cha mwili kumhusu. Lakini ukweli bado ni

ukweli. Hakuna mtu anayetaka kuzungumza kinyume na ukweli wa ukweli, kwa maana Ninapozungumza ni kuhusiana na ukweli; sio bahatisho, wala si unabii. Jua kwamba Mungu anaweza kuinuka kwa kiwango kikubwa, na, zaidi ya hayo, Anaweza kujificha katika vina virefu. Yeye ni Asiyefikirika na akili yako, Yeye ni Mungu wa viumbe vyote, na sio Mungu binafsi ambaye Amedhaniwa na mtu mmoja hasa.

Maono ya Kazi ya Mungu (3)

Mara ya kwanza ambapo Mungu alipata mwili ilikuwa kupitia kutungwa mimba kwa Roho Mtakatifu, na hili lilikuwa muhimu kwa kazi Aliyokusudia kufanya. Enzi ya Neema ilianza na Jina la Yesu. Wakati Yesu Alianza kufanya huduma Yake, Roho Mtakatifu Alianza kutoa ushuhuda kwa jina la Yesu, na jina la Yehova halikuzungumziwa tena, na badala yake Roho Mtakatifu Alianza kazi mpya hasa kwa jina la Yesu. Ushuhuda wa wale waliomwamini Yeye ulitolewa kwa ajili ya Yesu Kristo, na kazi waliyoifanya walifanya pia kwa ajili ya Yesu Kristo. Hitimisho Enzi ya Sheria ya Agano la Kale lilimaanisha kuwa kazi iliyofanywa hasa kutumia jina la Yehova ilikuwa imefikia kikomo. Baada ya hii, jina la Mungu halikuwa Yehova tena; badala yake Yeye Aliitwa Yesu, na kutoka hapa Roho Mtakatifu Alianza kazi hasa kwa kutumia jina la Yesu. Kwa hiyo leo, watu ambao leo bado hula na kunywa maneno ya Yehova, na bado hutumia kazi ya Enzi ya Sheria—je, hufuati masharti bila kufikiria? Je! Hujakwama katika siku za zamani? Leo, unajua kwamba siku za mwisho zimefika. Wakati Yesu atakapokuja, bado Ataitwa Yesu? Yehova aliwaambia watu wa Israeli kwamba Masihi angekuja, lakini alipofika, hakuitwa Masihi bali Yesu. Yesu alisema kwamba Angekuja tena, na kwamba Angekuja kama Alivyoondoka. Haya yalikuwa maneno ya Yesu, lakini je, ulishuhudia jinsi Yesu alivyoondoka? Yesu aliondoka akiwa juu ya wingu jeupe, lakini je, Yeye Mwenyewe angerudi kati ya binadamu juu ya wingu jeupe? Ingekuwa hivyo, je, si bado angeitwa Yesu? Wakati Yesu Atakuja tena, enzi itakuwa tayari imebadilika, je, hivyo bado Ataweza kuitwa Yesu? Je, Mungu Anajulikana tu kwa jina la Yesu? Je, hangeweza kuitwa kwa jina jipya katika enzi mpya? Je, sura ya mtu mmoja na hasa jina moja vinaweza kumwakilisha Mungu katika ukamilifu wake? Katika kila enzi, Mungu Anafanya kazi mpya na huitwa kwa jina jipya; Je, anawezaje kufanya kazi sawa katika enzi tofauti? Itakuwaje Yeye kugandamana na yale ya zamani? Jina la Yesu lilichukuliwa kuwa la kazi ya ukombozi, hivyo bado Yeye Anaweza kuitwa kwa jina moja wakati Atarudi katika siku za mwisho? Je, bado Yeye Atafanya kazi ya ukombozi? Ni kwa nini Yehova na Yesu ni kitu kimoja, ilhali wanaitwa kwa majina tofauti katika enzi hizi tofauti? Je, si kwa sababu enzi za kazi Yao ni tofauti? Jina moja linawezaje kumwakilisha Mungu kwa ukamilifu wake? Kwa njia hii, lazima Mungu aitwe kwa jina tofauti katika enzi tofauti, lazima Atumie jina kubadilisha enzi na kuwakilisha hiyo enzi, kwa kuwa hakuna jina moja linaweza kumwakilisha Mungu mwenyewe kikamilifu. Na kila jina linaweza tu kuwakilisha kipengele cha wakati cha tabia ya Mungu katika

enzi fulani; yote linahitaji kufanya ni kuwakilisha kazi Yake. Kwa hivyo, Mungu Anaweza kuchagua jina lolote ambalo linafaa tabia yake kuwakilisha enzi nzima. Bila kujali iwapo ni enzi ya Yehova, au ni enzi ya Yesu, kila enzi inawakilishwa kwa jina. Baada ya Enzi ya Neema, enzi ya mwisho imewadia na Yesu Amekwisha kuja. Itakuwaje awe bado anaitwa Yesu? Itakuwaje awe bado anachukua umbo la Yesu miongoni mwa watu? Je, umesahau kuwa Yesu Alikuwa tu sura ya Mnazareti? Je, umesahau kuwa Yesu Alikuwa tu mkombozi wa wanadamu? Itakuwaje achukue kazi ya kushinda na kurekebisha mwanadamu katika siku za mwisho? Yesu aliondoka akiwa juu ya wingu jeupe, huu ni ukweli, lakini Angewezaje kurudi juu ya wingu jeupe kati ya wanadamu na bado aitwe Yesu? Ikiwa Yeye kweli alikuja juu ya wingu, si Angetambuliwa na mwanadamu? Je, si watu ulimwenguni kote wangemtambua Yeye? Katika hali hiyo, je, si Yesu peke Yake ndiye angekuwa Mungu? Katika hali hiyo, sura ya Mungu ingekuwa ni sura ya Myahudi, na ingekuwa vilevile milele. Yesu alisema kwamba Angewasili kama Alivyoondoka, lakini unajua maana halisi ya maneno Yake? Je, angeweza kwa kweli kuwaambia ninyi kundi la watu? Unajua tu kwamba Atawasili kama Alivyoondoka juu ya wingu, lakini unajua hasa jinsi Mungu Mwenyewe hufanya kazi Yake? Ikiwa ungeweza kuona kweli, basi maneno ya Yesu yanapaswa kuelezwa vipi? Alisema: Wakati Mwana wa Adamu atakapokuja katika siku za mwisho, Yeye Mwenyewe hatajua, malaika hawatajua, wajumbe wa mbinguni hawatajua, na watu wote hawatajua. Baba tu ndiye atakayejua, yaani, Roho pekee ndiye atajua Hata Mwana wa Adamu Mwenyewe hajui, lakini wewe unaweza kuona na kujua? Ikiwa ungekuwa na uwezo wa kujua na kuona kwa macho yako mwenyewe, je, si maneno haya yatakuwa yalisemwa bure? Na Yesu alisema nini wakati huo? “Lakini juu ya hiyo siku na saa hiyo hakuna mtu anayejua, wala malaika wa mbinguni, isipokuwa Baba yangu tu. Lakini kama jinsi zilivyokuwa zile siku za Nuhu, ndivyo pia kuja kwa Mwana wa Adamu kutakuwa. ... Nanyi jiwekeni tayari, kwa kuwa saa msiyodhani ndipo atakapokuja Mwana wa Adamu.” Wakati siku hiyo itakapofika, Mwana wa Adamu Mwenyewe hatajua. Mwana wa Adamu inahusu umbo la Mungu lililopata mwili wa Mungu, ambaye atakuwa mtu wa kawaida. Hata Mwana wa Adamu mwenyewe hajui, kwa hiyo wewe ungejuaje? Yesu alisema kwamba Angewasili kama Alivyoondoka. Wakati Atakapowasili, hata Yeye Mwenyewe hajui, kwa hiyo Angekujulisha mapema? Je, unaweza kuona kuwasili kwake? Je, huo sio utani? Kila wakati ambao Mungu Atawasili hapa duniani, Yeye Atabadilisha jina lake, jinsia yake, mfano wake, na kazi yake; Yeye harudii kazi yake, na Yeye daima yu mpya na kamwe si wa zamani. Wakati Alikuwa hapo awali, Aliitwa Yesu; Je, anaweza bado kuitwa Yesu anapokuja tena wakati huu? Alipokuja hapo awali, Alikuwa wa kiume, Ataweza kuwa wa kiume tena wakati huu? Kazi Yake Alipokuja wakati wa Enzi ya Neema ilikuwa ya kusulubishwa msalabani; Atakapokuja tena, je, bado Atawakomboa wanadamu kutoka kwenye dhambi? Je, bado Atasulubishwa msalabani? Je, huko hakutakuwa kurudia kazi Yake? Je, hukujua kwamba Mungu daima ni mpya na kamwe si wa zamani? Kuna

wale ambao wanasema kuwa Mungu habadiliki. Hiyo ni sahihi, lakini inaashiria kutobadilika kwa tabia ya Mungu na kiini Chake. Mabadiliko ya jina lake na kazi hayathibitishi ya kuwa kiini chake kimebadilika; kwa maneno mengine, Mungu siku zote Atakuwa Mungu, na hii kamwe haitabadilika. Iwapo utasema kuwa kazi ya Mungu daima inabaki vile vile, basi Angekuwa na uwezo wa kumaliza mpango wake wa usimamizi wa miaka elfu sita? Wewe hujua tu kwamba Mungu habadiliki milele, lakini je, unajua kuwa Mungu ni mpya milele na kamwe si wa zamani? Kama kazi ya Mungu kamwe haikubadilika, basi Angeweza kulea mwanadamu hadi leo? Kama Mungu habadiliki, basi mbona Yeye tayari Amefanya kazi ya nyakati mbili? Kazi yake daima inaendelea mbele, na hivyo pia ndivyo tabia yake inafichuliwa kwa binadamu hatua kwa hatua, na kile ambacho kinafichuliwa ni tabia yake ya asilia. Hapo mwanzo, tabia ya Mungu ilikuwa siri kwa mwanadamu, na kamwe Yeye hadharani hakumfichulia mwanadamu tabia yake, na mwanadamu hakuwa na ufahamu kuhusu Yeye, na hivyo hatua kwa hatua Alitumia kazi Yake kumfichulia mwanadamu tabia Yake, lakini hii haina maana kuwa tabia Yake inabadilika katika kila enzi. Sio kweli kuwa tabia ya Mungu kila wakati inabadilika kwa ajili mapenzi Yake daima hubadilika. Bali, kwa kuwa enzi za kazi Yake ni tofauti, asili ya tabia Yake kwa ujumla hufichuliwa kwa binadamu hatua kwa hatua, ili mwanadamu aweze kumjua Yeye. Lakini hii si kwa njia yoyote ushahidi kuwa Mungu hapo awali hakuwa na tabia fulani na tabia Yake imebadilika hatua kwa hatua kwenye enzi zinazopita—ufahamu kama huo ni wenye kosa. Mungu humfichulia mwanadamu tabia yake fulani ya asili, kile Alichu, kwa mujibu wa enzi zinazopita. Kazi ya enzi moja haiwezi kueleza tabia nzima ya Mungu. Na kwa hivyo, maneno haya “Mungu daima ni mpya na kamwe si wa zamani” yanarejelea kazi yake, na maneno haya “Mungu habadiliki” kinarejelea kile ambacho Mungu anacho na alichu kiasili. Bila kujali, huwezi kubaini kazi ya miaka elfu sita kwa mtazamo mmoja, ama kwa kuielezea tu kwa maneno ambayo hayabadiliki. Huo ni ujinga wa mwanadamu. Mungu si wazi kama mwanadamu anavyofikiria, na kazi yake haitasimama katika enzi moja. Yehova, kwa mfano, haliwezi daima kusimamia jina la Mungu; Mungu pia hufanya kazi yake kwa kutumia Jina la Yesu, ambayo ni ishara ya vile ambavyo kazi ya Mungu daima husonga kwenda mbele.

Mungu siku zote huwa Mungu, na kamwe Yeye hatakuwa Shetani; Shetani daima ni Shetani, na yeye hawezi kuwa Mungu. Hekima ya Mungu, ajabu ya Mungu, haki ya Mungu, na adhama ya Mungu kamwe hayatabadilika. Kiini chake na anachomiliki na kile Anacho na alichu kamwe hakitabadilika. Kazi yake, hata hivyo, daima inaendelea mbele, daima inaenda ndani zaidi, kwa kuwa Mungu daima ni mpya na kamwe si wa zamani. Katika kila enzi Mungu huchukua jina jipya, katika kila enzi anafanya kazi mpya, na katika kila enzi Yeye huwaruhusu viumbe Wake kuona mapenzi Yake mapya na tabia Yake mpya. Ikiwa watu hawaoni dhihirisho la tabia mpya ya Mungu katika enzi mpya, wao si watamsulubisha msalabani milele? Na kwa

kufanya hivyo, si watakuwa wamebaini Mungu? Ikiwa Angepata mwili tu kama mume, watu wangemfafanua kama mume, kama Mungu wa wanaume, na kamwe hawangemwamini kuwa Mungu wa wanawake. Kisha, wanaume wangeamini kwamba Mungu ni wa jinsia sawa na wanaume, kwamba Mungu ni kichwa cha wanaume na je, wanawake? Hii si haki; je, huu sio utendeaji wa upendeleo? Ikiwa ingekuwa hivi, basi wale wote ambao Mungu aliwaokoa wangukuwa wanaume kama Yeye, na hakungekuwa na wokovu wa wanawake. Wakati ambapo Mungu aliumba wanadamu, Alimuumba Adamu na Akamuumba Hawa. Hakumuumba tu Adamu, lakini Aliwafanya wote mume na mke kwa mfano Wake. Mungu sio tu Mungu wa wanaume—Yeye pia ni Mungu wa wanawake. Mungu anafanya kazi mpya katika siku za mwisho. Atafichua tabia Yake zaidi, na haitakuwa huruma na upendo wa wakati wa Yesu. Kwa kuwa Ana kazi mpya, kazi hii mpya itaandamana na tabia mpya. Kwa hiyo kama kazi hii ingefanywa na Roho—kama Mungu hangepata mwili, na badala yake Roho angenena moja kwa moja kupitia radi ili mwanadamu hangukuwa na njia ya kuwasiliana na Yeye, je, mwanadamu angejua tabia yake? Kama Roho tu Angefanya kazi, basi mtu hangukuwa na njia yoyote ya kujua tabia Yake. Watu wanaweza tu kuona tabia ya Mungu kwa macho yao wenyewe wakati Anapopata mwili, wakati ambapo Neno laonekana katika mwili, na Anaonyesha tabia Yake yote kupitia mwili. Mungu kweli huishi kati ya wanadamu. Anaonekana; mwanadamu anaweza kweli kujihusisha na tabia Yake na kile Anacho na Alichu; ni kwa njia hii tu ndiyo mwanadamu anaweza kumjua kweli. Wakati huo huo, Mungu pia Amekamilisha kazi ya Mungu kuwa Mungu wa wanaume na wanawake, na Ametimiza ukamilifu wa kazi Yake katika mwili. Mungu harudii kazi yake katika kila enzi mpya. Kwa kuwa siku za mwisho zimewadia, Yeye Atafanya kazi ya siku za mwisho na kufichua tabia yake yote siku za mwisho. Siku za mwisho ni enzi tofauti, enzi ambayo Yesu Alisema lazima mteseke kwa maafu, na ukabiliwe na mitetemeko ya ardhi, njaa, na baa, ambavyo vitaonyesha kuwa hii ni enzi mpya, na sio tena Enzi ya Neema ya zamani. Kama, watu wanavyosema, Mungu daima habadiliki, tabia yake daima ni ya huruma na ya upendo, kwamba Yeye anampenda mwanadamu jinsi Anavyojipenda, na Anampa kila mwanadamu wokovu na kamwe hamchukii mwanadamu, basi Angekuwa na uwezo wa kukamilisha kazi yake? Wakati Yesu Alikuwa, Alisulubishwa msalabani, na Yeye Alijitoa kama sadaka kwa sababu ya wote wenye dhambi na kwa kujitoa Yeye mwenyewe madhabahuni. Yeye tayari Alikuwa Amemaliza kazi ya ukombozi na tayari Alikuwa Ametamatisha Enzi ya Neema, na hivyo ni nini kiini cha kurudia kazi ya enzi hiyo katika siku za mwisho? Je, kufanya kitu kimoja haitakuwa kukana kazi ya Yesu? Iwapo Mungu hatafanya kazi ya kusulubiwa awamu hii itakapofika, lakini Yeye Asalie mwenye mapenzi na Mungu wa huruma, je, anaweza kufikisha enzi hii mwisho? Je, Mungu mwenye upendo na mwenye huruma, si Angeweza kuhitimisha enzi hii? Katika kazi yake ya kuhitimisha enzi, tabia ya Mungu ni ile ya kuadibu na hukumu, ambayo inafichua yote ambayo si ya haki, na kuhukumu wanadamu hadharani, na kukamilisha wale

ambao wanampenda kwa ukweli. Ni tabia tu kama hii ndiyo ambayo inaweza kufikisha enzi hii mwisho. Siku za mwisho tayari zimewadia. Kila kitu kitatengashwa kulingana na aina, na kitagawanywa katika makundi tofauti kulingana na asili yake. Huu ni wakati ambapo Mungu Atafichua matokeo na hatima ya binadamu. Kama mwanadamu hatashuhudia kuadibu na hukumu yake, basi hakutakuwepo na mbinu ya kufichua uasi na udhalimu wao mwanadamu. Ni kwa njia ya kuadibu na hukumu ndipo mwisho wa mambo yote yatafunuliwa. Mwanadamu huonyesha tu ukweli ulio ndani yake anapoadibiwa na kuhukumiwa. Mabaya yataekwa na mabaya, mema na mema, na wanadamu watatenganishwa kulingana na aina. Kupitia kuadibu na hukumu, mwisho wa mambo yote utafichuliwa, ili mabaya yaadhibiwe na mazuri yatunukiwe zawadi, na watu wote watakuwa wakunyenyekwa chini ya utawala wa Mungu. Kazi hii yote inapaswa kutimizwa kupitia kuadibu kwa haki adhibu na hukumu. Kwa sababu upotovu wa mwanadamu umefika upeo wake na uasi wake umekua mbaya mno, ni haki ya tabia ya Mungu tu, ambayo hasa ni ya kuadibu na hukumu, na imefichuliwa kwa kipindi cha siku za mwisho, inayoweza kubadilisha na kukamilisha mwanadamu. Ni tabia hii pekee ambayo itafichua maovu na hivyo kuwaadhibu watu wote dhalimu. Kwa hivyo, tabia kama hii imejazwa umuhimu wa enzi, na ufunuo na maonyesho ya tabia yake ni kwa ajili ya kazi ya kila enzi mpya. Mungu hafichui tabia yake kiholela na bila umuhimu. Kama, wakati wa mwisho wa mwanadamu umefichuliwa katika kipindi cha siku za mwisho, Mungu bado anamfadhili binadamu kwa huruma na upendo usioisha, kama yeye bado ni wa kupenda mwanadamu, na kutompitisha mwanadamu katika hukumu ya haki, bali anamwonyesha stahamala, uvumilivu, na msamaha, kama bado Yeye anamsamehe mwanadamu bila kujali ubaya wa makosa anayofanya, bila hukumu yoyote ya haki: basi usimamizi wa Mungu ungetamatishwa lini? Ni wakati gani tabia kama hii itaweza kuwaongoza wanadamu katika hatima inayofaa? Chukua, kwa mfano, hakimu ambaye daima ni mwenye upendo, mwenye roho safi na mpole. Anawapenda watu bila kujali dhambi wanazozifanya, na ni mwenye upendo na stahamala kwa watu bila kujali hao ni nani. Kisha ni lini ambapo ataweza kufikia uamuzi wa haki? Katika siku za mwisho, ni hukumu ya haki tu inaweza kumtenganisha mwanadamu kulingana na aina yake na kumleta mwanadamu katika ufalme mpya. Kwa njia hii, enzi nzima inafikishwa mwisho kupitia kwa tabia ya Mungu iliyo ya haki ya hukumu na kuadibu.

Kazi ya Mungu kokote katika usimamizi wake ni wazi kabisa: Enzi ya Neema ni Enzi ya Neema, na siku za mwisho ni siku za mwisho. Kuna tofauti baina ya kila enzi, kwa kuwa katika kila enzi Mungu Anafanya kazi ambayo inawakilisha enzi hiyo. Ili kazi ya siku za mwisho iweze kufanywa, lazima kuwe na kuungua, hukumu, kuadibu, ghadhabu, na uharibifu wa kuleta enzi kwenye kikomo. Siku za mwisho zinaashiria enzi ya mwisho. Wakati wa enzi ya mwisho, je, Mungu si Ataleta enzi kwenye kikomo? Na ni kwa njia tu ya kuadibu na hukumu ndio inaweza

kuleta enzi kwenye kikomo. Ni kwa njia hii tu ndiyo Anaweza kuitamatisha enzi hiyo. Madhumuni ya Yesu yalikuwa kwamba mwanadamu aweze kuendelea kuwepo, kuishi, na kuweza kuwepo kwa njia bora zaidi. Alimwokoia mwanadamu kutoka kwa dhambi ili mwanadamu akome upotovu wa kudumu na kamwe asiishi katika Kuzimu na jahanamu, na kwa kumwokoia mwanadamu kutoka kwa Kuzimu na jahanamu, Yesu alimwezesha mwanadamu kuendelea kuishi. Sasa, siku za mwisho zimewadia. Mungu atamwagamiza mwanadamu, Atamharibu mwanadamu kabisa, ambayo ina maana kuwa Atageuza uasi wa binadamu. Kwa hivyo, huruma ya Mungu na tabia yake ya hapo zamani ya kupenda haitakuwa na uwezo wa kuhitimisha enzi hiyo, na haitakuwa na uwezo wa kukamilisha usimamizi wa Mungu wa miaka elfu sita. Kila enzi inaonyesha uwakilishi maalum wa tabia ya Mungu, na kila enzi ina kazi ambayo inafaa kufanywa na Mungu. Kwa hivyo, kazi iliyofanywa na Mungu mwenyewe kwa kila enzi ina dhihirisho la tabia Yake ya ukweli, na jina Lake na kazi anaofanya hubadilika na enzi—zote ni mpya. Wakati wa Enzi ya Sheria, kazi ya kumwelekeza mwanadamu ilifanyika katika Jina la Yehova, na awamu ya kwanza ya kazi ilifanyika duniani. Kazi ya awamu hii ilikuwa ni kujenga hekalu na madhabahu, na kutumia sheria kuwaongoza watu wa Israeli na kufanya kazi miongoni mwao. Kwa kuongoza watu wa Israeli, Alizindua kituo cha kazi Yake hapa duniani. Kwa msingi huu, Yeye Alipanua kazi yake nje ya Israeli, ambayo ni kusema kwamba, kuanzia Israeli, Aliendeleza kazi yake nje, ili vizazi vya baadaye walikuja kujua polepole kwamba Yehova Alikuwa Mungu, na kuwa Yehova Alikuwa Ameumba mbingu na nchi na vitu vyote, Alitengeneza viumbe vyote. Yeye Alieneza kazi yake kupitia kwa watu wa Israeli. Nchi ya Israeli ilikuwa ya mahali takatifu pa kwanza pa kazi ya Yehova hapa duniani, na kazi ya Mungu ya hapo mwanzoni ilikuwa kote katika nchi ya Israeli. Hiyo ilikuwa kazi ya Enzi ya Sheria. Wakati wa Enzi ya Neema, Yesu Alikuwa Mungu ambaye Alimwokoia mwanadamu. Alichokuwa nacho na Aliyekuwa ni neema, upendo, huruma, uvumilivu, subira, unyenyekevu, huduma, na stahamala, na nyingi ya kazi ambayo Alifanya ilikuwa kwa ajili ya kumwokoia mwanadamu. Tabia Yake ilikuwa ya huruma na upendo, na kwa sababu Yeye Alikuwa na huruma na upendo, ilikuwa sharti asulubishwe msalabani kwa ajili ya mwanadamu, ili kuonyesha kwamba Mungu Alimpenda mwanadamu jinsi anavyojipenda, kwa kiasi kwamba Yeye mwenyewe Alijitoa kama kafara na kwa ukamilifu Wake. Wakati wa Enzi ya Neema, jina la Mungu lilikuwa ni Yesu, ambalo lina maana kuwa Mungu Alikuwa Mungu ambaye Alimwokoia mwanadamu, na ya kwamba Alikuwa Mungu wa rehema na wa upendo. Mungu Alikuwa na mwanadamu. Upendo wake, huruma yake, na wokovu wake uliandamana na kila mtu. Mwanadamu angeweza tu kupata amani na furaha, kupokea baraka zake, kupokea neema yake kubwa na nyingi, na kupokea wokovu wake iwapo mwanadamu angekubali jina lake na akubali uwepo wake. Kupitia kusulubiwa kwa Yesu, wale wote ambao walimfuata Yeye walipokea wokovu na walisamehewa dhambi zao. Wakati wa Enzi ya Neema, jina la Mungu

lilikuwa ni Yesu. Kwa maneno mengine, kazi ya Enzi ya Neema ilifanywa hasa katika Jina la Yesu. Wakati wa Enzi ya Neema, Mungu Aliitwa Yesu. Yeye Alifanya kazi mpya zaidi ya Agano la Kale, na kazi yake ilimalizika kwa kusulubiwa, na ya kwamba huo ulikuwa ukamilifu wa kazi yake. Kwa hivyo, wakati wa Enzi ya Sheria Yehova ndilo lilikuwa jina la Mungu, na katika Enzi ya Neema jina la Yesu lilimwakilisha Mungu. Katika siku za mwisho, jina lake ni Mwenyezi Mungu—mwenye uweza, na yeye hutumia nguvu zake kumwongoza mwanadamu, kumshinda mwanadamu, kumtwaa mwanadamu, na mwishowe, kuhitimisha enzi hiyo. Katika kila enzi, katika awamu yote ya kazi yake, tabia ya Mungu ni dhahiri.

Hapo mwanzo, kumwongoza mwanadamu wakati wa Enzi ya Sheria ya Agano la Kale ilikuwa kama kuyaongoza maisha ya mtoto. Wanadamu wa mwanzoni sana walikuwa wazaliwa wapya wa Yehova, ambao walikuwa Waisraeli. Hawakuelewa jinsi ya kumcha Mungu au kuishi duniani. Ambayo ni kusema, Yehova aliwaumba wanadamu, yaani, Yeye aliwaumba Adamu na Hawa, lakini Hakuwapa uwezo wa kuelewa jinsi ya kumcha Yehova au kufuata sheria za Yehova duniani. Bila mwongozo wa moja kwa moja wa Yehova, hakuna ambaye angeweza kulijua hili moja kwa moja, kwani mwanzoni mwanadamu hakuwa na uwezo huo wa kuelewa. Mwanadamu alijua tu kwamba Yehova alikuwa Mungu, na hakuwa na habari ya namna ya kumcha Yeye, nini cha kufanya ili kumcha Yeye, kumcha Yeye na akili gani, na nini cha kutoa katika kumcha Yeye, mwanadamu alijua tu jinsi ya kufurahia kile ambacho kingeweza kufurahiwa kati ya viumbe wa Yehova, lakini mwanadamu hakuwa na fununu ya aina gani ya maisha duniani yalifaa yale ya kiumbe cha Mungu. Bila mtu wa kuwaelekeza, bila mtu wa kuwaongoza binafsi, wanadamu kama hao hawangeweza kamwe kuishi maisha ya kufaa wanadamu, na wangeweza tu kutekwa na Shetani kwa siri. Yehova aliwaumba wanadamu, ambayo ni kusema kwamba Yeye aliumba babu za wanadamu: Hawa na Adamu. Lakini hakuwapa akili zaidi au hekima. Ingawa walikuwa tayari wanaishi duniani, hawakuelewa takriban chochote. Na kwa hiyo, kazi ya Yehova ya kuwaumba wanadamu ilikuwa imefanyika nusu tu, haikuwa imekaribia kukamilika. Alikuwa ameumba tu mfano wa mwanadamu kutoka kwa udongo na kumpa pumzi Yake, lakini Hakuwa amempa mwanadamu radhi ya kutosha kumcha Yeye. Hapo mwanzo, mwanadamu hakuwa na akili ya kumcha Yeye, au kumwogopa Yeye. Mwanadamu alijua tu jinsi ya kuyasikiliza maneno Yake lakini hakujua ujuzi wa msingi wa maisha duniani na sheria za kawaida za maisha. Na kwa hiyo, ingawa Yehova aliumba mwanamume na mwanamke na kumaliza siku saba za shughuli, Hakukamilisha uumbaji wa mwanadamu hata kidogo, kwa maana mwanadamu alikuwa ganda tu, na hakuwa na uhalisi wa kuwa mwanadamu. Mwanadamu alijua tu kwamba ni Yehova aliyeumba wanadamu, lakini mwanadamu hakuwa na fununu ya jinsi ya kutii maneno na sheria za Yehova. Na kwa hiyo, baada ya kuumbwa kwa wanadamu, kazi ya Yehova ilikuwa mbali sana kumalizika. Pia

alitakiwa kuwaongoza wanadamu kabisa mbele Yake ili wanadamu waweze kuishi pamoja duniani na kumcha Yeye, na ili wanadamu waweze kwa mwongozo Wake kuingia katika njia sahihi ya maisha ya kawaida ya binadamu duniani baada ya kuongozwa na Yeye. Kwa njia hii tu ndiyo kazi ambayo ilikuwa imeendeshwa kwa kiasi kikubwa kupitia jina la Yehova ilimalizika kabisa; yaani, kwa njia hii tu ndiyo kazi ya Yehova ya kuumba ulimwengu ilihitimishwa kabisa. Na kwa hiyo, kwa vile Alimuumba mwanadamu, Alipaswa kuongoza maisha ya wanadamu duniani kwa miaka elfu kadhaa, ili wanadamu waweze kutii amri na sheria Zake, na kushiriki katika shughuli zote za maisha ya kufaa ya binadamu duniani. Wakati huo tu ndio kazi ya Yehova ilikamilika kabisa. Alianza kazi hii baada ya kuumba wanadamu, na kazi Yake iliendelea mpaka wakati wa Yakobo, wakati wana kumi na wawili wa Yakobo walipokuwa makabila kumi na mbili ya Israeli. Tangu wakati huo na kuendelea, kila mtu katika Israeli akawa watu walioongozwa rasmi na Yeye duniani, na Israeli ikawa mahali maalumu duniani ambapo Alifanya kazi Yake. Yehova aliwafanya watu hawa kundi la kwanza kati ya watu ambalo kwalo Alifanya kazi Yake rasmi duniani, na kuifanya nchi nzima ya Israeli kuwa kiwango cha kuanzia kazi Yake. Aliwatumia kama mwanzo wa hata kazi kubwa zaidi, ili watu wote waliozaliwa kutoka Kwake duniani wangejua jinsi ya kumcha Yeye na kuishi duniani. Na kwa hiyo, matendo ya Waisraeli yakawa mfano wa kufuatwa na Mataifa, na kile kilichosemwa kati ya watu wa Israeli kikawa maneno ya kusikizwa na Mataifa. Kwa kuwa walikuwa wa kwanza kupokea sheria na amri za Yehova, na vivyo hivyo pia walikuwa wa kwanza kujua jinsi ya kuzicha njia za Yehova. Wao walikuwa mababu wa binadamu ambao walijua njia za Yehova, na walikuwa wawakilishi wa wanadamu waliochaguliwa na Yehova. Enzi ya Neema ilipofika, Yehova hakuwaongoza wanadamu kwa namna hii tena. Mwanadamu alikuwa amefanya dhambi na kujiachia mwenyewe kwa dhambi, na kwa hiyo Akaanza kumwokoza mwanadamu kutoka kwa dhambi. Kwa njia hii, alimshutumu mwanadamu mpaka mwanadamu akakombolewa kabisa kutoka kwa dhambi. Katika siku za mwisho, mwanadamu ameshuka kwenye kiasi hicho cha upotovu mpaka kazi ya hatua hii inaweza kutelezwa tu kupitia hukumu na kuadibu. Ni kwa njia hii tu ndiyo kazi inaweza kufanikishwa. Hii imekuwa kazi ya enzi kadhaa. Kwa maneno mengine, Mungu hutumia jina Lake, kazi Yake, na taswira tofauti za Mungu kugawanya na kuhamisha enzi; jina la Mungu na kazi Yake vinawakilisha enzi Yake na kuwakilisha kazi Yake katika kila enzi. Kama kazi ya Mungu katika kila enzi ni sawa daima, naye daima anaitwa kwa jina sawa, ni jinsi gani basi mwanadamu atamjua Yeye? Mungu lazima aitwe Yehova, na mbali na Mungu kuitwa Yehova, yeyote ambaye ataitwa jina jingine si Mungu. Ama kwa njia nyingine Mungu Anaweza tu kuitwa Yesu, na Mungu hawezi kuitwa jina lingine isipokuwa Yesu; na mbali na Yesu, Yehova si Mungu, na wala Mwenyezi Mungu si Mungu. Mwanadamu anaamini kuwa ni ukweli Mungu ni mwenye uweza, lakini Mungu ni Mungu pamoja na mwanadamu; Sharti aitwe Yesu, kwa kuwa Mungu yu pamoja na mwanadamu. Kufanya hili ni kufuata

mafundisho, na kumshurutisha Mungu kwenye eneo fulani. Kwa hivyo, kazi ambayo Mungu hufanya katika kila enzi, jina ambalo Yeye huitwa, na mfano ambao Yeye hutwaa—kazi ambayo Yeye hufanya katika kila hatua mpaka leo—hivi havifuati kanuni hata moja, na hayakabiliwi na kikwazo chochote. Yeye ni Yehova lakini pia ni Yesu, na vile vile ni Masihi, na Mwenyezi Mungu. Kazi yake inaweza kubadilika polepole, na kuna mabadiliko sambamba katika jina lake. Hamna jina moja ambalo linaweza kumwakilisha Yeye kikamilifu, lakini majina yote ambayo Yeye huitwa yanaweza kumwakilisha Yeye, na kazi ambayo Amefanya katika kila enzi inawakilisha tabia yake. Tuseme, siku za mwisho zikifika, Mungu ambaye unamtazamia bado ni Yesu, na bado anaendesha wingu jeupe, na bado ana sura ya Yesu, na maneno ambayo Yeye anayasema ni bado maneno ya Yesu: “Mnapaswa kuwapenda jirani zenu kama mnavyoyipenda nyinyi wenyewe, mnapaswa kufunga na kuomba, wapende adui zenu kama mnavyopenda maisha yenu wenyewe, stahimili wengine, na muwe na uvumilivu na unyenyekevu. Lazima mfanye haya yote. Hapo tu ndipo mtaweza kuwa wafuasi Wangu. Mkifanya haya yote, mtaweza kuingia katika Ufalme Wangu.” Je, hii haitakuwa kazi ya Enzi ya Neema? Je, hii haitakuwa njia ambayo ilizungumziwa katika Enzi ya Neema? Mnajisikiaje mnaposikia maneno haya. Je, hamhisi kuwa bado hii ni kazi ya Yesu? Je, hayo hayatakuwa marudio ya kazi Yake? Je, hii inaweza kumpendeza mwanadamu? Mnaweza kuhisi kuwa kazi ya Mungu inaweza kubaki tu kama ilivyo sasa, na haiwezi kuendelea zaidi. Yeye ana nguvu kubwa kiasi hiki pekee, na hana kazi mpya ya kutekeleza, na Amefikia upeo wake. Miaka elfu mbili iliyopita ilikuwa ni Enzi ya Neema, na miaka elfu mbili baadaye, Yeye bado anahubiri kwa njia ya Enzi ya Neema, na bado anawafanya wanadamu watubu. Watu watasema “Mungu, una nguvu kubwa kiasi hiki pekee. Niliamini kuwa wewe ni mwenye busara sana, ilhali unajua tu uvumilivu na unashughulika na subira tu,. Unajua tu jinsi ya kupenda adui yako na bila chochote kingine.” Katika akili ya mwanadamu, Mungu milele Atakuwa Alivyokuwa katika Enzi ya Neema, na mwanadamu daima ataamini ya kwamba Mungu ni wa upendo na rehema. Je, unafikiri kuwa kazi ya Mungu daima itapitia kwenye ardhi ile ile ya zamani? Na hivyo, katika awamu hii ya kazi yake Yeye hawezi kusulubishwa, na kila kitu mnachoona na kugusa kitakuwa tofauti na chochote ambacho mmewahi kufikiri na kusikia. Leo, Mungu hashiriki na Mafarisayo, Anauweka ulimwengu katika ujinga, na ninyi wafuasi tu ndio mnamjua Yeye, kwa maana Yeye hatazulubiwa tena. Wakati wa enzi ya Neema, Yesu alihubiri waziwazi kote katika nchi kwa ajili ya kazi Yake ya injili. Alijishughulisha na Mafarisayo kwa ajili ya kusulubiwa; kama Hangejishughulisha na Mafarisayo na wale waliokuwa mamlakani hawangejua kamwe juu Yake, Angewezaje kushutumiwa, na kisha kusalitiwa na kupigiliwa misumari msalabani? Na kwa hiyo, Alijishughulisha na Mafarisayo kwa ajili ya kusulubiwa. Leo, Yeye hufanya kazi Yake kwa siri ili kuepuka majaribu. Kazi, umuhimu, na mandhari ya kupata mwili kwa Mungu kuwili vyote vilikuwa tofauti, kwa hiyo kazi Aliyoifanya ingewezaje kuwa sawa kabisa?

Je, Jina la Yesu—"Mungu pamoja nasi,"—linaweza kuwakilisha tabia ya Mungu kwa ukamilifu wake? Je, linaweza kueleza Mungu kwa ukamilifu? Kama mwanadamu atasema ya kwamba Mungu Ataitwa tu Yesu, na hawezi kuwa na jina lingine kwa sababu Mungu hawezi kubadilisha tabia yake, basi maneno hayo ni kufuru! Je, unaamini kwamba jina la Yesu, Mungu pamoja nasi, linaweza kumwakilisha Mungu kikamilifu? Mungu Anaweza kuitwa majina mengi, lakini baina ya majina haya mengi, hamna moja ambalo linaweza kujumlisha yote ambayo Mungu Anamiliki, na hamna jina moja ambalo linaweza kumwakilisha Mungu kikamilifu. Na hivyo Mungu Ana majina mengi, lakini majina haya mengi hayawezi kuelezea tabia ya Mungu kikamilifu, kwa kuwa tabia ya Mungu ni tajiri sana, na yanazidi uwezo wa mwanadamu kumjua Yeye. Lugha ya mwanadamu haina uwezo wa kumfafanua Mungu kwa ukamilifu. Mwanadamu ana msamiati finyu tu ambao anaweza kufafanua yote anayojua kuhusu tabia ya Mungu: kubwa, yenye heshima, ya ajabu, isiyoeleweka, kuu, takatifu, yenye haki, yenye hekima, na kadhalika. Maneno mengi sana! Msamiati kama huo finyu hauwezi kuelezea kile kidogo mtu ameshuhudia juu ya tabia ya Mungu. Baadaye, watu wengi waliongeza maneno zaidi ili kueleza vizuri zaidi ari ndani ya mioyo yao: Mungu ni mkuu sana! Mungu ni mtakatifu sana! Mungu ni wa kupendeza sana! Leo, maneno kama haya yamefikia kilele chake, lakini bado mwanadamu hawezi kujieleza wazi wazi. Na kwa hiyo, kwa mwanadamu, Mungu ana majina mengi, lakini Hana jina moja, na hilo ni kwa sababu nafsi ya Mungu ni ya ukarimu sana, na lugha ya mwanadamu haitoshi sana. Neno au jina moja maalum halina uwezo wa kumwakilisha Mungu kwa ukamilifu wake. Kwa hivyo, je, Mungu Anaweza kuchukua jina moja lisilobadilika? Mungu ni mkuu sana na mtakatifu sana, kwa hivyo mbona wewe huwezi kumruhusu Yeye abadili jina Lake katika kila enzi mpya? Kwa hivyo, katika kila enzi ambayo Mungu binafsi hufanya kazi yake mwenyewe, Yeye hutumia jina ambalo linafaa enzi hiyo ili kujumlisha kazi ambayo anaifanya. Yeye hutumia hili jina haswa, ambalo linamiliki umuhimu wa wakati, kuwakilisha tabia yake katika enzi hiyo. Mungu hutumia lugha ya mwanadamu kuelezea tabia yake mwenyewe. Hata hivyo, watu wengi ambao wamepata uzoefu wa kiroho na wamemuona Mungu binafsi bado wanahisi kuwa jina moja maalumu haliwezi kumwakilisha Mungu kwa ukamilifu wake—ole wetu, hili linasikitisha, hivyo mwanadamu hamwiti Mungu kwa jina lolote, lakini humwita tu "Mungu." Moyo wa mwanadamu unaonekana kujawa na upendo, lakini pia unaonekana kuzongwa na ukinzani, kwa maana mwanadamu hajui jinsi ya kumueleza Mungu. Kile Mungu alichoko ni cha ukarimu sana kiasi kwamba hakuna kabisa njia ya kukieleza. Hakuna jina moja ambalo linaweza kutoa muhtasari wa tabia Ya Mungu, na hakuna jina moja ambalo linaweza kuelezea yote ambayo Mungu anacho na Alichoko. Kama mtu ataniuliza, "Ni jina gani hasa unalotumia?" Nitamwambia, "Mungu ni Mungu!" Je, hilo silo jina bora zaidi la Mungu? Je, huko sio kufafanua bora zaidi kuhusu tabia ya Mungu? Hali ikiwa hivi, kwa nini mnatumia juhudi nyingi sana kutafuta jina la Mungu? Kwa nini ufikirie sana, kukaa bila kula na kulala, kwa ajili ya jina? Siku itawadia

ambapo Mungu hataitwa Yehova, Yesu, au Masihi—Yeye Ataitwa tu Muumba. Wakati huo, majina yote ambayo Alichukua hapa duniani yatafikia kikomo, kwa kuwa kazi yake hapa duniani itakuwa imefika mwisho, na baada ya hapo Mungu hatakuwa na jina. Wakati mambo yote yatakuja kuwa chini ya utawala wa Muumba, kwa nini umwite kwa jina sahihi ila bado halijakamilika? Je, bado unatafuta jina la Mungu sasa? Je, bado unathubutu kusema kuwa Mungu Anaitwa tu Yehova? Je, bado unathubutu kusema kuwa Mungu Anaweza tu kuitwa Yesu? Je, unaweza kubeba dhambi ya kumkufuru Mungu? Unapaswa kujua kuwa Mungu mwanzoni hakuwa na jina. Yeye Alichukua tu jina moja, au majina mawili, ama majina mengi kwa sababu Alikuwa na kazi ya kufanya na Alikuwa na jukumu la kumsimamia mwanadamu. Jina lolote ambalo anaitwa Yeye, je, si lile analolichagua kwa hiari yake? Je, Yeye atakuhitaji wewe, mmoja wa viumbe wake Wake, kuliamua? Jina ambalo Mungu Anaitwa ni kwa mujibu wa kile ambacho mwanadamu anaweza kufahamu na lugha ya mwanadamu, lakini hili jina haliwezi kujumlishwa na mwanadamu. Wewe unaweza kusema tu kuwa mbinguni kuna Mungu, ya kwamba Yeye anaitwa Mungu, na kwamba Yeye mwenyewe ni Mungu mwenye nguvu nyingi, busara tele, wakuinuliwa sana, wa ajabu kuu, mwenye siri kuu, mwenye uweza mkuu sana, na huwezi kusema mengi zaidi; hayo ndiyo yote unayoyajua. Kwa njia hii, je, jina la Yesu tu linaweza kumwakilisha Mungu mwenyewe? Wakati siku za mwisho zitawadia, ingawa ni Mungu ndiye anafanya kazi yake, ni sharti jina lake libadilike, kwa kuwa ni enzi tofauti.

Mungu akiwa mkuu zaidi katika ulimwengu wote, na katika ulimwengu wa juu, Angeweza kujieleza Mwenyewe kwa ukamilifu kwa kutumia mfano wa mwili? Mungu hujivika Mwenyewe mwili ili kufanya hatua ya kazi Yake. Hakuna umuhimu mahsusi kwa sura ya mwili, na haina uhusiano na kupita kwa enzi, na haina uhusiano wowote na tabia ya Mungu. Kwa nini Yesu hakuruhusu sura Yake kubaki? Kwa nini hakumruhusu mtu kuchora sura Yake, ili iweze kupitishwa kwa vizazi vya baadaye? Kwa nini Hakuruhusu watu kukubali kwamba sura yake ilikuwa sura ya Mungu? Ingawa sura ya mwanadamu iliumbwa kwa mfano wa Mungu, ni kwa jinsi gani sura ya mwanadamu ingewakilisha mfano wa Mungu aliyeinuliwa? Mungu anapopata mwili, Yeye anashuka tu kutoka mbinguni na kuingia ndani ya mwili maalumu. Roho Wake ashuka kingia ndani ya mwili, kwa njia ambayo Yeye hufanya kazi ya Roho. Roho huonyesha katika mwili, na Roho hufanya kazi Yake katika mwili. Kazi iliyofanyika katika mwili inawakilisha Roho kwa ukamilifu, na mwili ni kwa ajili ya kazi, lakini hilo halimaanishi kwamba sura ya mwili ni mbadala wa sura halisi ya Mungu Mwenyewe; hili silo kusudi na umuhimu wa Mungu kupata mwili. Anapata mwili tu ili Roho apate mahali pa kuishi Akifanya kazi Yake, ili Apate kufanikisha kazi Yake katika mwili, ili watu waweze kuona matendo Yake, waelewe tabia Yake, kusikia maneno Yake, na kujua ajabu ya kazi Yake. Jina Lake linawakilisha tabia Yake, kazi Yake inawakilisha utambulisho Wake, lakini Hajawahi kusema kuwa kuonekana Kwake

katika mwili kunawakilisha sura Yake; hiyo ni fikira tu ya mwanadamu. Na kwa hiyo, hoja muhimu za kupata mwili kwa Mungu ni jina Lake, kazi Yake, tabia Yake, na jinsia Yake. Yeye hutumia hivi kuwakilisha usimamizi wake katika enzi hii. Kuonekana Kwake katika mwili hakuna uhusiano na usimamizi Wake, na ni kwa ajili tu ya kazi Yake wakati huo. Hata hivyo haiwezekani kwa Mungu mwenye mwili kutokuwa na kuonekana maalumu, na kwa hiyo Anachagua jamii inayofaa ili kuamua kuonekana Kwake. Ikiwa kuonekana kwa Mungu kuna umuhimu wa uwakilishi, basi wale wote ambao wana sifa muhimu za uso sawa na Zake pia wanawakilisha Mungu. Hilo silo kosa la kupita kiasi? Picha ya Yesu ilichorwa na mwanadamu ili mwanadamu angeweza kumwabudu. Wakati huo, hakuna maagizo maalum yaliyotolewa na Roho Mtakatifu, na kwa hiyo mwanadamu alipitisha picha hiyo iliyodhaniwa hadi leo. Kwa kweli, kulingana na kusudi la Mungu, mwanadamu hakupaswa kufanya hivyo. Ni ari tu ya mwanadamu ambayo imesababisha picha ya Yesu kubaki hadi siku hii. Mungu ni Roho, na mwanadamu hataweza kamwe kuwa na uwezo wa kutoa muhtasari wa hasa sura Yake ni nini. Sura Yake inaweza tu kuwakilishwa na tabia Yake. Huwezi kufafanua kuonekana kwa pua Lake, kwa mdomo Wake, kwa macho Yake, na kwa nywele Zake. Wakati ufunuo ulipofika kwa Yohana, aliona sura ya Mwana wa Adamu: Kutoka mdomoni mwake ulikuwa upanga mkali ukatao kuwili, macho Yake yalikuwa kama miale ya moto, kichwa Chake na nywele vilikuwa vyeupe kama sufu, miguu Yake ilikuwa kama shaba iliyong'arishwa, na kulikuwa na mshipi wa dhahabu unaozunguka kifua Chake. Ingawa maneno yake yalikuwa wazi sana, sura ya Mungu alioieleza haikuwa sura ya kiumbe. Aliyoona ni maono tu, na sio sura ya mtu kutoka ulimwengu yakinifu. Yohana alikuwa ameona maono, lakini hakuwa ameshuhudia kuonekana kwa kweli kwa Mungu. Sura ya mwili wa Mungu uliopata mwili ni sura ya uumbaji, na haiwezi kuwakilisha tabia ya Mungu kwa ukamilifu wake. Wakati Yehova alipoumba wanadamu, Alisema kuwa Alifanya hivyo kwa mfano Wake na Akaumba mume na mke. Wakati huo, Alisema Alifanya mume na mke katika mfano wa Mungu. Ingawa sura ya mwanadamu inafanana na sura ya Mungu, haimaanishi kuwa kuonekana kwa mwanadamu ni sura ya Mungu. Huwezi kutumia lugha ya mwanadamu kufanya muhtasari wa sura ya Mungu kwa ukamilifu, kwa maana Mungu ameinuliwa sana, ni mkubwa sana, wa ajabu sana na Asiyeleweka!

Wakati Yesu Alikuwa kufanya kazi yake, ilikuwa ni kwa uongozi wa Roho Mtakatifu; Yeye Alitenda vile ambavyo Roho Mtakatifu Alitaka, na haikuwa kwa mujibu wa Enzi ya sheria ya Agano la Kale ama kwa mujibu wa kazi ya Yehova. Ingawa kazi ambayo Yesu Alikuwa kufanya haikuambatana na sheria za Yehova ama amri za Yehova, chanzo chao kilikuwa sawa. Kazi ambayo Yesu Alifanya iliwakilisha jina la Yesu, na iliwakilisha Enzi ya Neema; kazi iliyofanywa na Yehova, iliwakilisha Yehova, na iliwakilisha Enzi ya Sheria. Kazi yao ilikuwa kazi ya Roho mmoja katika enzi tofauti. Kazi ambayo Yesu Alifanya ingeweza tu kuwakilisha

Enzi ya Neema, na kazi ambayo Yehova Alifanya ingeweza tu kuwakilisha Enzi ya Sheria ya Agano la Kale. Yehova Aliwaongoza tu watu wa Israeli na Misri, na mataifa yote nje ya Israeli. Kazi ya Yesu katika Enzi ya Neema ya Agano Jipya ilikuwa kazi ya Mungu katika jina la Yesu kwa kuwa Yesu ndiye Aliongoza enzi hii. Iwapo utasema kuwa kazi ya Yesu ilikuwa kwa msingi wa kazi ya Yehova, na kuwa hakufanya kazi yoyote mpya, na kuwa yote Aliyofanya ilikuwa kwa mujibu wa maneno ya Yehova, kulingana na kazi ya Yehova na unabii wa Isaya, basi Yesu hakuwa Mungu Aliyekuwa katika mwili. Kama Alitekeleza kazi yake kwa njia hii, basi Yeye Alikuwa mtume au mfanyikazi wa Enzi ya Sheria. Iwapo ni kama unavyosema, basi Yesu hangeweza kuzindua enzi, wala hangeweza kufanya kazi nyingine. Kwa njia hiyo hiyo, Roho Mtakatifu ni sharti afanye kazi Yake hasa kupitia kwa Yehova, na isipokuwa kupitia kwa Yehova Roho Mtakatifu hangeweza kufanya kazi yoyote mpya. Mwanadamu amekosea kwa kuona kazi ya Yesu kwa njia hii. Kama mwanadamu anaamini kwamba kazi iliyofanywa na Yesu ilifanywa inaambatana na maneno ya Yehova na unabii wa Isaya, basi, je, Yesu Alikuwa Mungu Aliyepata mwili, au Yeye Alikuwa nabii? Kwa mujibu wa mtazamo huu, hakukuwa na Enzi ya Neema, na Yesu hakuwa Mungu Aliyepata mwili, kwa kuwa kazi ambayo Alifanya haingeweza kuwakilisha Enzi ya Neema na ingewakilisha tu Enzi ya Sheria ya Agano la Kale. Kungekuwepo tu na enzi mpya wakati Yesu Alikuwa kufanya kazi mpya, Alipozindua enzi mpya, na kupenya katika kazi iliyokuwa imefanyika hapo awali katika nchi ya Israeli, na hakufanya kazi yake kwa mujibu wa kazi iliyofanywa na Yehova huko Israeli, hakuzingatia sheria Yake ya zamani, na hakufuata kanuni zozote, na Alifanya kazi mpya ambayo Alitakiwa kufanya. Mungu Mwenyewe anakuja kuzindua enzi, na Mungu mwenyewe huja kuleta enzi kwenye kikomo. Mwanadamu hana uwezo wa kufanya kazi ya kuanzisha enzi hiyo na kuhitimisha enzi. Kama Yesu hakuleta kazi ya Yehova kwenye kikomo baada ya Yeye kuja, basi hio inadhihirisha ya kwamba Yeye Alikuwa tu mwanadamu, na hakuwakilisha Mungu. Kwa usahihi kwa sababu Yesu Alikuwa na kuhitimisha kazi ya Yehova, Akaendeleza kazi ya Yehova na, aidha, Akatekeleza kazi Yake, kazi mpya, inathibitisha kuwa hii ilikuwa enzi mpya, na kwamba Yesu alikuwa Mungu Mwenyewe. Walifanya kazi katika awamu mbili zinazotofautiana. Awamu moja ilifanyika katika hekalu, na hiyo nyingine ilifanyika nje ya hekalu. Awamu moja ilikuwa ya kuongoza maisha ya mwanadamu kwa mujibu wa sheria, na awamu nyingine ilikuwa ya kutoa kafara ya dhambi. Awamu hizi mbili za kazi bila shaka zilikuwa tofauti; huu ni mgawanyiko wa enzi ya zamani na enzi mpya, na hakuna kosa kusema kuwa hizo ni enzi mbili! Maeneo ya kazi yao yalikuwa tofauti, na kiini cha kazi yao kilikuwa tofauti, na lengo la kazi yao lilikuwa tofauti. Kwa hivyo, enzi hizi zinaweza kugawanywa kwa awamu mbili: Agano la Kale na Jipya, ambayo ni kusema, enzi mpya na ya zamani. Yesu alipokuja hakuenda katika hekalu, ambayo inathibitisha kwamba enzi ya Yehova ilikuwa imeisha. Hakuungia hekaluni kwa sababu kazi ya Yehova katika hekalu ilikuwa imekamilika, na haikuhitajika kufanywa tena, na kwa hiyo

kuifanya tena kungekuwa kuirudia. Kwa kuondoka tu hekaluni, kuanza kazi mpya na kuzindua njia mpya nje ya hekalu, ndio Aliweza kuifikisha kazi ya Mungu kwa upeo wake. Kama Hangeenda nje ya hekalu kufanya kazi Yake, kazi ya Mungu haingeweza kamwe kuendelea mbele kupita hekalu, na hakungekuwa na mabadiliko yoyote mapya. Na kwa hiyo, Yesu Alipokuja, Hakuingia hekaluni, na Hakufanya kazi Yake hekaluni. Alifanya kazi Yake nje ya hekalu, na Akafanya kazi Yake kwa uhuru Akiandamana na wanafunzi. Kuondoka kwa Mungu katika hekalu kufanya kazi Yake kulikuwa na maana kwamba Mungu alikuwa na mpango mpya. Kazi Yake ilikuwa ifanyike nje ya hekalu, na ilikuwa iwe kazi mpya ambayo haingezuiliwa kwa njia ya utekelezaji wake. Kuwasili kwa Yesu kulimaliza kazi ya Yehova ya wakati wa Agano la Kale. Ingawa ziliitwa kwa majina mawili tofauti, awamu zote mbili za kazi zilifanywa na Roho mmoja, na kazi ya pili ilikuwa mwendelezo wa kazi ya kwanza. Kwa kuwa jina lilikuwa tofauti, na kiini cha kazi kilikuwa tofauti, basi enzi ilikuwa tofauti. Wakati Yehova Alikuwa, hiyo ilikuwa enzi ya Yehova, na wakati Yesu Alikuwa, hiyo ilikuwa enzi ya Yesu. Na kwa hivyo, kila wakati Mungu Anapokuja, anaitwa kwa jina moja, Yeye anawakilisha enzi moja, na Yeye anazindua njia mpya; na kwa kila njia mpya, Yeye huchukua jina jipya, ambalo inaonyesha kuwa Mungu daima ni mpya na wala si wa zamani, na ya kwamba kazi yake daima inasonga mbele. Historia inasonga mbele daima, na kazi ya Mungu inasonga mbele daima. Ili mpango wa usimamizi wa Mungu wa miaka elfu sita ufike upeo wake, lazima uendeleo kusonga mbele. Kila siku ni sharti Yeye afanye kazi mpya, kila mwaka lazima Yeye afanye kazi mpya, ni sharti Yeye azindue njia mpya, azindue enzi mpya, aanzishe kazi mpya na kubwa zaidi, na ni sharti alete majina mapya na kazi mpya. Roho wa Mungu daima hufanya kazi mpya, na kamwe Hashikili njia za zamani au masharti. Kazi Yake pia kamwe haikomi, na inatendeka wakati wote. Ukisema kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ni isiyobadilika, basi kwa nini Yehova aliwaruhusu makuhani kumhudumia Yeye hekaluni, lakini Yesu hakuvingia hekaluni licha ya ukweli kwamba Alipokuja watu pia walisema kwamba Alikuwa kuhani mkuu, na kwamba Alikuwa wa nyumba ya Daudi na pia kuhani mkuu, na Mfalme mkuu? Na kwa nini Hakutoa dhabihu? Kuingia hekaluni au la—hii yote sio kazi ya Mungu Mwenyewe? Iwapo, kama mwanadamu anavyofikiria, Yesu Atakuja, akiwa anaitwa Yesu wakati wa siku za mwisho, na bado juu ya wingu jeupe, akishuka miongoni mwa wanadamu kwa mfano wa Yesu: huko hakutakuwa kurudia kazi yake? Je, si Roho Mtakatifu Atakuwa Ameshikamana na ya kale? Yote yale ambayo mwanadamu anaamini ni mawazo, na yote ambayo mwanadamu anakubali ni kulingana na maana halisi, na ni kwa mujibu wa mawazo yale; yanakinzana na kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu, na hayafuatani na nia ya Mungu. Mungu pia hawezi kufanya hivyo; Mungu si mpumbavu na mjinga kiasi hicho, na kazi Yake si rahisi kama unavyofikiria. Kwa kutegemeza mambo yote yanayofikiriwa na mwanadamu, Yesu Atarejea juu ya wingu na Atateremka kati yenu. Mtamwona Yeye ambaye, akiwa amepaa juu ya wingu, atawaambia kwamba yeye ni Yesu. Nanyi pia mtatazama alama za

misumari katika mikono yake, na mtamjua Yeye ni Yesu. Naye ndiye Atakayewaokoa tena, na Atakuwa Mungu wenu Mwenye nguvu. Yeye ndiye Atakayewaokoa, na kuwakabidhi ninyi jina jipya, na kumpa kila mtu jiwe jeupe, ambapo baadaye mtakubaliwa kuingia katika ufalme wa mbinguni na kulakiwa kwenye paradiso. Je, imani kama hizo si fikira za mwanadamu? Je, Mungu hufanya kazi kulingana na fikira za mwanadamu, au, je, Yeye hufanya kazi kinyume cha fikira za mwanadamu? Je, si fikira zote za mwanadamu zatoka kwa Shetani? Je, mwanadamu hajapotoshwa na Shetani? Kama Mungu Alifanya kazi yake kulingana na fikira ya mwanadamu, je, si Mungu Angekuwa Shetani? Je, si Angekuwa wa aina sawa na viumbe Wake wenyewe? Kwa kuwa viumbe Wake wamepotoshwa na Shetani hadi mwanadamu amekuwa mfano halisi ya Shetani, kama Mungu Angefanya kazi kwa mujibu wa vitu vya Shetani, si angekuwa katika ligi ya Shetani. Mwanadamu anawezaje kupima kina cha kazi ya Mungu? Na kwa hivyo, Mungu hafanyi kazi kwa mujibu wa fikira ya mwanadamu, na hangefanya kazi kwa njia unazofikiria. Kuna wale ambao husema kwamba Mungu mwenyewe Alisema kuwa Atawasili kwa wingu. Ni ukweli kuwa Mungu mwenyewe Alisema hivyo, lakini, je, hujui kuwa siri za Mungu haziwezi kueleweka na mwanadamu? Je, unajua kuwa maneno ya Mungu hayawezi kuelezwa na mwanadamu? Na wewe una hakika, bila tashwishi yoyote, kuwa ulipewa nuru na kuangaziwa na Roho Mtakatifu? Je, si Roho Mtakatifu Aliyekuonyesha moja kwa moja kwa namna hii? Je, haya ni maelekezo ya Roho Mtakatifu, au ni fikira zako? Ulisema, “Haya yalisemwa na Mungu mwenyewe.” Lakini hatuwezi kutumia fikira zetu na akili zetu kupima maneno ya Mungu. Na kuhusu maneno ya Isaya, je, unaweza kueleza maneno yake kwa kujiamini kikamilifu? Je, wewe unathubutu kueleza maneno yake? Kwa sababu huthubutu kueleza maneno ya Isaya, mbona unathubutu kueleza maneno ya Yesu? Nani ameinuliwa kuliko mwingine, Yesu au Isaya? Kwa vile jibu ni Yesu, kwa nini unaeleza maneno yaliyosemwa na Yesu? Je, Mungu Angeweza kukwambia kuhusu kazi yake mapema? Hakuna kiumbe kinachoweza kufahamu, wala hata wajumbe walio mbinguni, wala hata Mwana wa Adamu, kwa hivyo wewe ungejua? Mwanadamu ana upungufu mkuu. Kilicho muhimu kwenu sasa ni kufahamu awamu tatu za kazi. Kutoka kwa kazi ya Yehova mpaka ile ya Yesu, na kutoka kwa kazi ya Yesu hadi kwa kazi iliyoko kwa awamu hii ya sasa, awamu hizi tatu zinajumlisha upana wote wa usimamizi wa Mungu, na zote ni kazi za Roho mmoja. Kutoka Alipoumba ulimwengu, Mungu Amekuwa Akisimamia wanadamu. Yeye ndiye Mwanzo na ndiye Mwisho; Yeye ndiye wa Kwanza na wa Mwisho, na Yeye ndiye mwanzilishi wa enzi na Yeye ndiye huleta enzi kwenye kikomo. Awamu tatu za kazi, katika enzi tofauti na maeneo mbalimbali, hakika yanafanywa na Roho mmoja. Wote ambao wanatenganisha awamu hizi tatu wanampinga Mungu. Sasa, lazima uelewe kwamba kazi yote kutoka awamu ya kwanza hadi leo ni kazi ya Mungu mmoja, ni kazi ya Roho mmoja, ambapo hakuna shaka.

Kuhusu Biblia (1)

Biblia inapaswa kuangaliwaje kuhusiana na imani kwa Mungu? Hili ni swali muhimu sana. Kwa nini tunawasiliana swali hili? Kwa sababu wakati ujao utaeneza injili na kupanua kazi ya Enzi ya Ufalme, na haitoshi tu kuweza kuzungumza juu ya kazi ya Mungu leo. Ili kupanua kazi Yake, ni muhimu zaidi kwamba unakuwa na uwezo wa kubadilisha dhana za watu za dini ya kale na njia za kale za imani, na kuwaacha wakiwa wameshawishika kabisa—na kufikia katika hoja hiyo Biblia inahusishwa. Kwa miaka mingi, imani ya watu ya kitamaduni (hiyo ya Ukristo, moja ya dini kuu tatu za dunia) imekuwa ni kusoma Biblia; kujitenga na Biblia sio imani kwa Bwana, kujitenga na Biblia ni kufuata imani tofauti tofauti na uzushi, na hata pale watu wanaposoma vitabu vingine, msingi wa vitabu hivi ni lazima uwe ni ufafanuzi wa Biblia. Ni kusema kwamba, kama unasema unamwamini Bwana, basi ni lazima usome Biblia, unapaswa kula na kunywa Biblia, na nje ya Biblia hupaswi kuabudu kitabu kingine ambacho hakihusishi Biblia. Ikiwa utafanya hivyo, basi unamsaliti Mungu. Kuanzia kipindi ambapo kulikuwa na Biblia, imani ya watu kwa Bwana imekuwa imani katika Biblia. Badala ya kusema watu wanamwamini Bwana, ni bora kusema kwamba wanaamini Biblia; badala ya kusema wameanza kusoma Biblia, ni bora kusema wameanza kuamini Biblia; na badala ya kusema wamerudi mbele ya Bwana, ingekuwa vyema kusema wamerudi mbele ya Biblia. Kwa njia hii, watu wanaibudu Biblia kana kwamba ni Mungu, kana kwamba ni damu yao ya uzima na kuipoteza itakuwa ni sawa na kupoteza maisha yao. Watu wanaitazama Biblia kuwa ni kuu kama Mungu, na hata kuna wale wanaoiona kuwa ni kuu kuliko Mungu. Kama watu hawatakuwa na kazi ya Roho Mtakatifu, ikiwa hawawezi kuhisi Mungu, wanaweza kuendelea kuishi—lakini punde tu watakapoipoteza Biblia, au kupoteza sura na maneno maarufu sana kutoka katika Biblia, basi inakuwa ni kana kwamba wamepoteza maisha yao. Na hivyo, pale ambapo watu wataanza kumwamini Bwana wanaanza kusoma Biblia, na kuikariri Biblia, na kadri ya sehemu kubwa ya Biblia wanayoweza kukariri, ndivyo hii inathibitisha kwamba wanampenda Bwana na ni watu wenye imani kuu. Wale ambao wameisoma Biblia na wanaweza kuizungumzia kwa wengine wote ni kaka na dada wazuri. Kwa miaka yote hii, imani ya watu na uaminifu kwa Bwana vimepimwa kulingana na kiwango cha ufahamu wao wa Biblia. Watu wengi hawaelewi kwa nini wanapaswa kumwamini Mungu, wala jinsi ya kumwamini Mungu, na hawafanyi chochote zaidi ya kutafuta kiupofu dondoo ili kufasiri sura za Biblia. Watu hawajawahi kufuata mwelekeo wa kazi ya Roho Mtakatifu; muda wote huo, hawajafanya chochote, bali kujifunza na kuchunguza Biblia kwa papara, na hakuna hata mmoja ambaye amepata kazi mpya ya Roho Mtakatifu nje ya Biblia, hakuna ambaye amewahi kujitenga na Biblia, wala kuthubutu kujitenga na Biblia. Watu wamejifunza Biblia kwa miaka yote hii, wamekuja na maelezo mengi sana, na kufanya kazi kubwa sana, pia wana maoni mengi tofauti kuhusu Biblia, ambayo yamekuwa ni mdahalo

usiokwisha, kiasi kwamba ziadi ya madhehebu elfu mbili yameanzishwa hadi leo. Wote wanataka kutafuta ufafanuzi maalumu, au siri za kina zaidi katika Biblia, wanataka kuichunguza, na kuipata katika usuli wa kazi ya Yehova katika Israeli, au usuli wa kazi ya Yesu katika Yudea, au siri nyingi zaidi ambazo hakuna yeyote anayejua. Watu wanavyoichukulia Biblia ni shauku na imani, na hakuna anayeweza kufafanua kikamilifu kisa cha ndani au kiini cha Biblia. Kwa hivyo, leo watu bado wana hisia zisizoelezeka za kimiujiza linapokuja suala la Biblia, na hata wana shauku nayo zaidi, na wanaiamini hata zaidi. Leo, kila mtu anataka kutafuta unabii wa kazi ya siku za mwisho katika Biblia, wanataka kugundua ni kazi gani Mungu hufanya wakati wa siku za mwisho na kuna ishara gani ya siku za mwisho. Kwa njia hii, kuabudu kwao Biblia kunakuwa na maana sana, na kadri wanaposogelea siku za mwisho, ndivyo wanavyozidi kuonyesha imani pofu kwa unabii wa Biblia, hususani ule wa siku za mwisho. Kwa imani hiyo ya upofu katika Biblia, kwa imani hiyo katika Biblia, hawana shauku ya kutafuta kazi ya Roho Mtakatifu. Katika dhana za watu, wanadhani kwamba ni Biblia pekee ndiyo inayoweza kuleta kazi ya Roho Mtakatifu; ni katika Biblia pekee ndimo wanamoweza kupata nyayo za Mungu; ni katika Biblia pekee ndimo kulimofichika siri za kazi ya Mungu; ni kwenye Biblia pekee—na sio katika vitabu vinginevyo au watu—wanaoweza kufafanua kila kitu cha Mungu na ujumla wa kazi Yake; Biblia inaweza kuleta kazi ya mbinguni duniani; na Biblia inaweza kuanzisha na kuhitimisha enzi. Kwa dhana hizi, watu hawana shauku kutafuta kazi ya Roho Mtakatifu. Hivyo, licha ya kiasi gani Biblia ilikuwa ina msaada mkubwa kwa watu wa wakati wa nyuma, imekuwa ni kikwazo katika kazi ya Mungu ya hivi karibuni. Bila Biblia, watu wanaweza kutafuta nyayo za Mungu mahali kwingineko, bado leo, nyayo zake zimejumuishwa na Biblia, na kupanua kazi Yake ya hivi karibuni, imekuwa na ugumu mara mbili, na mapambano magumu. Hii yote ni kwa sababu ya sura na misemo maarufu kutoka katika Biblia, vilevile unabii mbalimbali wa Biblia. Biblia imekuwa sanamu katika akili za watu, limekuwa ni fumbo katika akili zao, na hawawezi kabisa kuamini kwamba Mungu anaweza kufanya kazi nje ya Biblia, hawawezi kuamini kwamba watu wanaweza kumpata Mungu nje ya Biblia, achilia mbali kuwa na uwezo wa kuamini kwamba Mungu angeweza kujitenga na Biblia wakati wa kazi ya mwisho na kuanza upya. Hili suala haliingii akilini mwa watu; hawawezi kuliadini, na wala hawawezi kulifikiria. Biblia imekuwa kikwazo kikubwa kwa watu kukubali kazi mpya ya Mungu, na imefanya kuwa vigumu kwa Mungu kuipanua kazi hii mpya. Hivyo, kama hamwelewi kisa cha ndani ya Biblia, hamtaweza kueneza injili kwa mafanikio, wala hamtaweza kuwa na ushuhuda wa kazi mpya. Ingawa, leo, hamsomi Biblia, bado ni maridhia katika Biblia, ambapo ni sawa na kusema, Biblia inaweza isiwe mikononi mwenu, lakini dhana zenu nyingi zinatoka humo. Huelewi asili ya Biblia au kisa cha ndani kuhusu hatua mbili za awali kuhusu kazi ya Mungu. Ingawa hamnywi na kula Biblia, mnapaswa kuielewa Biblia, mnapaswa kupata maarifa sahihi ya Biblia, na ni kwa njia hii tu ndipo mtaweza kujua mpango wa kazi ya Mungu ya usimamizi ya miaka 6000 inahusiana na nini

hasa. Mtatumia mambo haya kuwapata watu, kuwafanya wakiri kwamba mkondo huu ni njia ya kweli, kuwafanya wakiri kwamba, njia mnayoiendea leo, ni njia ya kweli, ambayo inaongozwa na Roho Mtakatifu, na haijawahi kufunguliwa na mwanadamu mwingine yeyote.

Baada ya Mungu kufanya kazi ya Sheria, Agano la Kale lilibuniwa, na ni hapo ndipo watu walianza kusoma Biblia. Baada ya Yesu kukuja, alifanya kazi ya Neema, na mitume Wake waliliandika Agano Jipya. Hivyo ndivyo Agano la Kale na Agano Jipya ya Biblia yalibuniwa, na hata leo, wale wote wanaomwamini Mungu wamekuwa wakisoma Biblia. Biblia ni kitabu cha historia. Ni kweli, pia kinahusisha baadhi ya unabii wa manabii, na unabii huu, kwa namna yoyote ile si historia. Biblia inajumuisha sehemu kadhaa—sio unabii tu, au kazi ya Yehova tu, wala hakuna nyaraka za Paulo pekee. Unapaswa kujua ni sehemu ngapi ambazo Biblia inajumuisha; Agano la Kale linajumuisha Mwanzo, Kutoka..., na pia kuna vitabu vya unabii ambavyo manabii waliandika. Mwishoni, Agano la Kale linakamilika kwa kitabu cha Malaki. Linarekodi kazi ya Enzi ya Sheria, ambayo iliongozwa na Yehova; kuanzia Mwanzo hadi Kitabu cha Malaki, ni rekodi kamilifu ya kazi ya Enzi ya Sheria. Ni sawa na kusema, Agano Jipya linarekodi yote ambayo yalipitiwa na watu ambao waliongozwa na Yehova katika Enzi ya Sheria. Wakati wa Enzi ya Sheria ya Agano la Kale, idadi kubwa ya manabii iliinuliwa na Yehova, walizungumza unabii kwa niaba Yake, walitoa maelekezo kwa makabila mbalimbali na mataifa, na wakatoa unabii juu ya kazi ambayo Yehova angefanya. Watu hawa ambao wameinuliwa wote walipewa na Yehova Roho ya unabii: Waliweza kutazama njozi kutoka kwa Yehova, na kusikia sauti Yake, na hivyo walivuviwa Naye na wakaandika unabii. Kazi waliyoifanya ilikuwa udhihirisho wa sauti ya Yehova, udhihirisho wa unabii wa Yehova, na kazi ya Yehova wakati huo ilikuwa ni kuwaongoza watu kwa njia ya Roho Mtakatifu; Hakufanyika mwili, na watu hawakuona uso Wake. Hivyo, aliwainua manabii wengi kufanya kazi Yake, na akawapatia mashauri ambayo waliyapelekea katika kila kabila na ukoo wa Israeli. Kazi yao ilikuwa ni kusema unabii, na baadhi yao waliandika maelekezo ya Yehova kwa ajili yao ili kuwaonesha wengine. Yehova aliwainua watu hawa kuzungumza unabii, kutoa unabii wa kazi ya wakati ujao au kazi ambayo ilikuwa bado haijafanyika wakati huo, ili kwamba watu wangepewe kutazama maajabu na hekima ya Yehova. Vitabu hivi vya unabii vilikuwa tofauti kabisa na vitabu vingine vya Biblia; yalikuwa ni maneno yaliyozungumzwa au kuandikwa na wale waliopewa Roho ya unabii—na wale ambao walipata njozi au sauti kutoka kwa Yehova. Kuacha vitabu vya unabii, kila kitu kingine katika Agano la Kale ni rekodi zilizochukuliwa na watu baada ya Yehova kukamilisha kazi Yake. Vitabu hivi haviwezi kusimama badala ya unabii uliozungumzwa na manabii walioinuliwa na Yehova, kama ambavyo Mwanzo na Kutoka haviwezi kulinganishwa na Kitabu cha Isaya na Kitabu cha Danieli. Unabii ulikuwa unazungumzwa kabla ya kazi haijafanyika; wakati huo, vitabu vingine viliandikwa baada ya

kuwa kazi imemalizika, kazi ambayo watu walikuwa wanaiweza. Manabii wa wakati huo walivuviwa na Yehova na kuzungumza unabii, walizungumza maneno mengi, na walitoa unabii wa mambo ya Enzi ya Neema, na vilevile uharibifu wa dunia katika siku za mwisho—kazi ambayo Yehova alipanga kufanya. Vitabu vilivyosalia vyote vinarekodi kazi iliyofanywa na Yehova katika Israeli. Hivyo, unaposoma Biblia, unakuwa unasoma kile ambacho Yehova alifanya katika Israeli; Biblia ya Agano la Kale kimsingi inarekodi kazi ya Mungu ya kuwaongoza Israeli, kumtumia Musa kuwaongoza Waisraeli kutoka Misri, aliyewaondoa katika shida za Farao, na kuwachukua na kuwapeleka jangwani, ambapo baada ya hapo wakaingia Kaanani na kila kitu baada ya hapa ilikuwa ni kuanza maisha yao Kaanani. Yote, isipokuwa hii ni rekodi za kazi ya Yehova katika Israeli yote. Kila kitu kilichorekodiwa katika Agano la Kale ni kazi ya Yehova katika Israeli, ni kazi Aliyofanya Yehova katika nchi ambapo Aliwaumba Adamu na Hawa. Kuanzia wakati ambapo Mungu alianza rasmi kuwaongoza watu duniani baada ya Nuhu, yote ambayo yamerekodiwa katika Agano la Kale ni kazi ya Israeli. Na kwa nini hakuna kazi yoyote iliyorekodiwa ambayo ni nje ya Israeli? Kwa sababu nchi ya Israeli ni chimbuko la binadamu. Mwanzoni hakukuwa na nchi yoyote tofauti na Israeli, na Yehova hakufanya kazi katika sehemu nyingine yoyote. Kwa namna hii, kile kilichorekodiwa katika Agano la Kale la Biblia ni kazi ya Mungu katika Israeli pekee wakati huo. Maneno yaliyozungumzwa na manabii, na Isaya, Danieli, Yeremia na Ezeieli ... maneno yao yanatabiri kazi Yake nyingine duniani, yanatabiri kazi ya Yehova Mungu Mwenyewe. Yote haya yalitoka kwa Mungu, ilikuwa ni kazi ya Roho Mtakatifu, na tofauti na vitabu hivi vya manabii, mambo mengine yote ni rekodi ya uzoefu wa watu juu ya kazi ya Yehova wakati huo.

Kazi ya uumbaji ilitokea kabla ya binadamu kuwepo, lakini Kitabu cha Mwanzo kilikuja tu baada ya kuwepo binadamu; kilikuwa ni kitabu kilichoandikwa na Musa wakati wa Enzi ya Sheria. Ni kama vitu vilivyotokea miongoni mwenu leo: Baada ya kutokea, mnayaandika ili kuwaonyesha watu katika maisha ya baadaye, na kwa watu wa baadaye, mliyoyarekodi ni mambo yaliyotokea wakati uliopita—na si chochote zaidi ya historia. Mambo yaliyorekodiwa katika Agano la Kale ni kazi ya Yehova katika Israeli, na kile kilichorekodiwa katika Agano Jipya ni kazi ya Yesu katika Enzi ya Neema; ni rekodi ya kazi iliyofanywa na Mungu katika enzi mbili tofauti. Agano la Kale linarekodi kazi ya Mungu wakati wa Enzi ya Sheria, na hivyo Agano la Kale ni kitabu cha kihistoria, wakati Agano Jipya ni zao la kazi ya Enzi ya Neema. Wakati kazi mpya ilipoanza, hii pia ilipitwa na wakati—na hivyo, Agano Jipya pia ni kitabu cha kihistoria. Kimsingi Agano Jipya halina mpangilio mzuri kama Agano la Kale, wala halirekodi mambo mengi. Maneno yote mengi yaliyozungumzwa na Yehova yamerekodiwa katika Agano la Kale la Biblia, ambapo baadhi tu ya maneno ya Yesu yamerekodiwa katika Injili Nne. Ni kweli, Yesu pia alifanya kazi nyingi sana, lakini haikurekodiwa kwa kina. Mambo machache

yamerekodiwa katika Agano Jipya ni kwa sababu ya kiasi cha kazi ambayo Yesu aliifanya; kiwango cha kazi Yake katika miaka mitatu na nusu duniani na kazi ile ya mitume ilikuwa ni pungufu zaidi kuliko kazi ya Yehova. Na hivyo, kuna vitabu vichache zaidi katika Agano Jipya kuliko Agano la Kale.

Biblia ni kitabu cha aina gani? Agano la Kale ni kazi ya Mungu katika Enzi ya Sheria. Agano la Kale la Biblia linarekodi kazi yote ya Yehova wakati wa Enzi ya Sheria na kazi Yake ya uumbaji. Lote linarekodi kazi iliyofanywa na Yehova, na hatimaye linahitimisha maelezo ya kazi ya Yehova kwa kitabu cha Malaki. Agano la Kale linarekodi kazi mbili zilizofanywa na Mungu: Moja ni kazi ya uumbaji, na nyingine ni kuamrisha sheria. Zote ni kazi zilizofanywa na Yehova. Enzi ya Sheria inawakilisha kazi chini ya jina la Yehova Mungu; ni ujumla wa kazi iliyofanywa kimsingi chini ya jina la Yehova. Hivyo, Agano la Kale linarekodi kazi ya Yehova, na Agano Jipya linarekodi kazi ya Yesu, kazi ambayo kimsingi ilifanywa chini ya jina la Yesu. Umuhimu wa jina la Yesu na kazi Aliyoifanya imerekodiwa sanasana katika Agano Jipya. Wakati wa Agano la Kale Enzi ya Sheria, Yehova alijenga hekalu na madhabahu katika Israeli, Aliongoza maisha ya Waisraeli duniani, kuzingatia kwamba walikuwa watu Wake, kundi la kwanza la watu ambalo alilichagua duniani na ambao walikuwa wanautafuta moyo Wake, kundi la kwanza ambalo Yeye Mwenyewe aliliongoza; ni sawa na kusema, makabila kumi na mawili ya Israeli walikuwa ni wateule wa kwanza wa Yehova, na hivyo siku zote Alifanya kazi ndani yao, hadi ambapo kazi ya Yehova ya Enzi ya Sheria ilihitimishwa. Hatua ya pili ya kazi ilikuwa ni kazi ya Enzi ya Neema ya Agano Jipya, na ilifanyika kati ya watu wa Kiyahudi, kati ya mojawapo ya makabila kumi na mawili ya Israeli. Mawanda ya kazi hii yalikuwa madogo kwa sababu Yesu alikuwa Mungu aliyepata mwili. Yesu alifanya kazi katika eneo lote la Yudea pekee, na Alifanya tu kazi ya miaka mitatu na nusu; hivyo, kile kilichorekodiwa katika Agano la Kale kiko mbali zaidi kupitiliza kiwango cha kazi kilichorekodiwa katika Agano la Kale. Kazi ya Yesu ya Enzi ya Neema kimsingi imerekodiwa katika Injili Nne. Njia iliyopitiwa na watu wa Enzi ya Neema ilikuwa ile mabadiliko ya juu juu katika tabia yao ya maisha, nyingi zaidi ambayo imerekodiwa katika nyaraka. Nyaraka zinaonyesha jinsi ambavyo Roho Mtakatifu alifanya kazi wakati huo. (Ni kweli, licha ya ama Paulo aliadibiwa au alikutana na majanga, katika kazi aliyofanya alikuwa ameelekezwa na Roho Mtakatifu, alikuwa ni mtu aliyetumiwa na Roho Mtakatifu wakati huo; Petro pia, alitumiwa na Roho Mtakatifu, lakini hakufanya kazi kubwa kama aliyofanya Paulo. Ingawa kazi ya Paulo ilikuwa na uchafu wa mwanadamu, kwa kuangalia nyaraka zilizoandikwa na Paulo, inaweza kuonekana ni jinsi gani Roho Mtakatifu alifanya kazi wakati huo; njia ambayo Paulo aliiongoza ilikuwa njia njema, ilikuwa ni sahihi, na ilikuwa ni njia ya Roho Mtakatifu.)

Ikiwa unatamani kuiona kazi ya Enzi ya Sheria, na kuona jinsi gani Waisraeli waliifuata

njia ya Yehova, basi ni lazima usome Agano la Kale; ikiwa unatamani kuelewa kazi ya Enzi ya Neema, basi ni lazima usome Agano Jipya. Lakini unawezaje kuona kazi ya siku za mwisho? Ni lazima ukubali uongozi wa Mungu wa leo, na kuingia katika kazi ya leo, maana hii ni kazi mpya na hakuna ambaye ameirekodi katika Biblia hapo nyuma. Leo, Mungu amefanyika mwili, na Amewachagua wateule wengine katika nchi ya China. Mungu anafanya kazi ndani ya watu hawa, Anaendelea na kazi Yake duniani, Anaendelea kutoka katika kazi ya Enzi ya Neema. Kazi ya leo ni njia ambayo mwanadamu hajawahi kuiendea, na njia ambayo hakuna mtu ambaye amewahi kuiona. Ni kazi ambayo haijawahi kufanywa hapo kabla—ni kazi ya Mungu ya hivi karibuni kabisa duniani. Hivyo, kazi ambayo haijawahi kufanywa kabla sio historia, kwa sababu sasa ni sasa, na bado haijawa muda uliopita. Watu hawajui kwamba Mungu amefanya kazi kubwa, mpya duniani, na nje ya Israeli, yaani imevuka mawanda ya Israeli, na zaidi ya unabii wa manabii, ambayo ni kazi mpya na ya kushangaza nje ya unabii, na kazi mpya kabisa nje ya Israeli, na kazi ambayo watu hawawezi kuelewa au kufikiria. Inawezekanaje Biblia kuwa na rekodi za wazi za kazi kama hiyo? Ni nani ambaye angeweza kurekodi kila hatua ya kazi ya leo, bila kuondoa kitu? Ni nani angeweza kurekodi kazi hii kubwa na yenye hekima ambayo inakataa maagano ya kitabu cha kale? Kazi ya leo sio historia, na kama vile, ikiwa unatamani kutembea katika njia ya leo, basi mnapaswa kutengana na Biblia, unapaswa kwenda mbele zaidi ya vitabu vya unabii au historia ya Biblia. Baada ya hapo tu ndipo utaweza kutembea njia mpya vizuri, na baada ya hapo ndipo utaweza kuingia katika ufalme mpya na kazi mpya. Unapaswa kuelewa ni kwa nini leo unaambiwa usisome Biblia, kwa nini kuna kazi nyingine ambayo inajitenga na Biblia, kwa nini Mungu haonekani mpya na wa kina zaidi katika Biblia, kwa nini badala yake kuna kazi kubwa zaidi nje ya Biblia. Haya ndiyo yote mnayopaswa kuelewa. Unapaswa kuelewa tofauti kati ya kazi ya zamani na kazi mpya, na hata kama hausomi Biblia, unapaswa kuitenganisha; kama hautaweza, bado utakuwa unaiabudu Biblia, na itakuwa ni vigumu sana kwako kuingia katika kazi mpya na kupitia mabadiliko mapya. Kwa kuwa kuna njia ya juu, kwa nini mjifunze hiyo ya chini, njia ya kale? Kwa kuwa kuna matamshi mapya, na kazi mpya, kwa nini uishi katikati ya rekodi za kale za kihistoria? Matamshi mapya yanaweza kukupa, ambayo yanathibitisha kwamba hii ni kazi mpya; rekodi za kale haziwezi kukushibisha, au kutosheleza mahitaji yako ya sasa, kitu ambacho kinathibitisha kwamba ni historia, na sio kazi ya hapa na sasa. Njia ya juu zaidi ni njia mpya zaidi, na kazi mpya, bila kujali njia ya zamani ni ya juu kiasi gani, bado ni historia ya kumbukumbu ya watu, na haijalishi ina thamani kiasi gani kama rejeleo, bado ni njia ya kale. Ingawa imerekodiwa katika “kitabu kitakatifu,” njia ya kale ni historia; ingawa hakuna rekodi yake katika “kitabu kitakatifu,” njia mpya ni ya hapa na sasa. Kwa njia hii inaweza kukuokoa, na kwa njia hii inaweza kukubadilisha, maana hii ni kazi ya Roho Mtakatifu.

Mnapaswa kuelewa Biblia—kazi hii ni ya umuhimu mkubwa sana! Leo, unapaswa kusoma

Biblia, maana hakuna jipya ndani yake; yote ni ya kale. Biblia ni kitabu cha kihistoria, na ikiwa ungekula na kunywa Agano la Kale wakati wa Enzi ya Neema—ikiwa ungeweka katika vitendo kile kilichokuwa kinatakiwa katika wakati wa Agano la Kale wakati wa Enzi ya Neema—Yesu angekukataa, na kukuhukumu; ikiwa ungetumia Agano la Kale katika kazi ya Yesu, basi ungekuwa Farisayo. Ikiwa, leo, utaweka pamoja Agano Jipya na la Kale kula na kunywa, na kuliweka katika vitendo, basi Mungu wa leo Atakuhukumu; utakuwa umebaki nyuma ya kazi ya leo ya Roho Mtakatifu! Ikiwa unakula na kunywa Agano la Kale na Agano Jipya, basi upo nje ya mkondo wa Roho Mtakatifu! Wakati wa kipindi cha Yesu, Yesu aliwaongoza Wayahudi na wale wote ambao walimfuata Yeye kulingana na kazi ya Roho Mtakatifu katika Yeye wakati huo. Hakuichukulia Biblia kama msingi wa kile Alichofanya, bali Alizungumza kulingana na kazi Yake; Hakutilia maanani kile ambacho Biblia ilisema, wala hakutafuta katika Biblia njia ya kuongoza wafuasi Wake. Kuanzia pale Alipoanza kufanya kazi, Aliongoza njia ya toba—neni ambalo halikutajwa kabisa katika unabii wa Agano la Kale. Sio kwamba tu Hakutenda kulingana na Biblia, lakini pia Aliongoza njia mpya, na Akafanya kazi mpya. Na wala Hakurejelea kabisa Biblia Alipohubiri. Wakati wa Enzi ya Sheria, hakuna ambaye aliweza kufanya miujiza Yake ya kuponya wagonjwa na kutoa mapepo. Hivyo, pia, kazi Yake, mafundisho Yake, na mamlaka na nguvu za maneno Yake yalizidi mtu yeyote wakati wa Enzi ya Sheria. Yesu alifanya tu kazi Yake mpya, na ingawa watu wengi walimhukumu kwa kutumia Biblia—na hata wakatumia Agano la Kale kumsulubisha—kazi Yake ilipitiliza Agano la Kale; kama hii haikuwa hivyo, kwa nini watu walimwangika msalabani? Ilikuwa ni kwa sababu haikusema kitu katika Agano la Kale la mafundisho Yake, na uwezo Wake wa kuponya wagonjwa na kutoa mapepo? Kazi Yake ilikuwa ni kwa ajili ya kuongoza katika njia mpya, haikuwa ni kwa makusudi ya kufanya ugomvi dhidi ya Biblia, au kwa makusudi kujitenga na Agano la Kale. Alikuwa tu kufanya huduma Yake, kuleta kazi mpya kwa wale waliomtamani sana na kumtafuta. Hakuja kufafanua Agano la Kale au kutetea kazi yake. Kazi Yake bado haikuwa ni kwa ajili ya kuruhusu Enzi ya Sheria kuendelea kukua, maana kazi Yake haikuzingatia Biblia kama msingi wake; Yesu alikuja kufanya tu kazi ambayo Alipaswa kufanya. Hivyo, Hakufafanua unabii wa Agano la Kale, wala Hakufanya kazi kulingana na maneno ya Enzi ya Sheria ya Agano la Kale. Alipuuzia kile ambacho Agano la Kale lilisema, Hakujalia kama lilikubaliana na kazi Yake au la, na Hakujali kile ambacho watu wengine walijua kuhusu kazi Yake, au namna walivyokuwa wakiihukumu. Aliendelea tu kufanya kazi ambayo Alipaswa kufanya, ingawa watu wengi walitumia unabii waliosema manabii wa Agano la Kale kumhukumu. Ilionekana kwa watu kana kwamba kazi Yake haikuwa na msingi, na kulikuwa na mengi ambayo yalikuwa hayapatani na rekodi za Agano la Kale. Je, haya hayakuwa makosa ya mwanadamu? Je, kuna haja ya kutumia mafundisho ya dini katika kazi ya Mungu? Je, ni lazima iwe kulingana na maneno ya unabii waliyosema manabii? Hata hivyo, kipi ni kikubwa: Mungu au Biblia? Kwa nini ni lazima kazi ya

Mungu iwe kulingana na Biblia? Je, inaweza kuwa kwamba Mungu hana haki ya kuwa juu ya Biblia? Je, Mungu hawezi kujitenga na Biblia na kufanya kazi nyingine? Kwa nini Yesu na wanafunzi Wake hawakutunza Sabato? Ikiwa Angetunza Sabato na matendo mengine kulingana na amri za Agano la Kale, kwa nini Yesu Hakutunza Sabato baada ya kuja, lakini badala yake Aliitawadha miguu, Akafunika kichwa, Akavunja mkate, na kunywa divai? Je, sio kwamba haya yote hayapatikani katika amri za Agano la Kale? Ikiwa Yesu aliliheshimu Agano la Kale, kwa nini Aliyakataa mafundisho haya. Unapaswa kujua ni kipi kilitangulia, Mungu au Biblia! Kuwa Bwana wa Sabato, je, Asingeweza pia kuwa Bwana wa Biblia?

Kazi iliyofanywa na Yesu wakati wa Agano Jipya ilifungua kazi mpya: Hakufanya kazi kulingana na kazi ya Agano la Kale, wala Hakutumia maneno yaliyozungumzwa na Yehova wa Agano la Kale. Alifanya kazi yake mwenyewe, na Alifanya kazi mpya zaidi, na kazi ambayo ilikuwa ya juu kuliko sheria. Hivyo, Alisema: “Msidhani ya kwamba Nilikuja kuiharibu torati au manabii; Sikuja kuharibu, bali kutimiliza.” Hivyo, kulingana na kile Alichokitimiza, mafundisho mengi yalikuwa yamevunjwa. Siku ya Sabato Alipowachukua wanafunzi wake kuenda katika shamba la nafaka, walichuma na kula masuke: Alikuwa Anaivunja Sabato, na Akasema, “Mwana wa Adamu ndiye Bwana hata wa siku ya sabato.” Kwa wakati huo, kulingana na sheria za Waisraeli, yeyote ambaye alikuwa haitunzi Sabato angepigwa na mawe hadi kufa. Hata hivyo Yesu, wala Hakuingia hekaluni wala Hakuitunza Sabato, na kazi Yake haikuwa imefanywa na Yehova wakati wa Agano la Kale. Hivyo, kazi aliyoifanya Yesu inapita sheria ya Agano la Kale, ilikuwa ni ya juu kuipita, na haikuwa na ulinganifu nayo. Wakati wa Enzi ya Neema, Yesu hakufanya kazi kulingana na sheria ya Agano la Kale, Aliyakataa mafundisho hayo. Lakini Waisraeli waliishikilia Biblia vikali na wakamshutumu Yesu—je, huku hukuwa kuikataa kazi ya Yesu? Leo, dunia ya dini pia inaishikilia Biblia vikali, na watu wengine husema, “Biblia ni kitabu kitakatifu, na inapaswa kusomwa.” Baadhi ya watu husema, “Kazi ya Mungu inapaswa itetewe milele, Agano la Kale ni agano la Mungu na Waisraeli, na haliwezi kubadilishwa, na Sabato inapaswa kutunzwa siku zote!” Je, hawa sio wapuuzi? Kwa nini Yesu Hakutunza Sabato? Je, Alikuwa Anafanya dhambi? Nani anaweza kuelewa mambo hayo? Haijalishi jinsi watu wanavyoisoma Biblia, itakuwa ni vigumu kuijua kazi ya Mungu kwa kutumia uwezo wao wa ufahamu. Hawatapata maarifa halisi ya Mungu, na fikira zao zitakuwa za ujinga kupita kiasi, kiasi kwamba wataanza kumpinga Mungu. Kama ingekuwa sio kwa ajili ya Mungu kupata mwili leo, watu wangeangamizwa na fikira zao wenyewe, na wangekufa katikati ya kuadibu kwa Mungu.

Kuhusu Biblia (2)

Biblia pia huitwa Agano la Kale na Agano Jipya. Je, mnajua “agano” linarejelea nini?

“Agano” katika Agano la Kale linatokana na makubaliano ya Yehova na watu wa Israeli Alipowaua Wamisri na kuwaokoa Waisraeli kutoka kwa Farao. Bila Shaka, uthibitisho wa haya makubaliano ulikuwa damu ya mwanakondoo iliyopakwa kwenye lintu, kupitia kwayo Mungu Alianzisha agano na mwanadamu, moja ambalo ilisemwa kuwa wale wote waliokuwa na damu ya mwanakondoo juu na pembeni mwa viunzi vya mlango walikuwa Waisraeli, walikuwa wateuliwa wa Mungu, na wote wangeokolewa na Yehova (kwa kuwa Yehova wakati ule Alikuwa karibu kuwaua wazaliwa wa kwanza wa kiume wa Misri wote na wazaliwa wa kwanza wa kondoo na ng’ombe). Agano hili lina viwango viwili vya maana. Hakuna mmoja wa watu au wanyama wa Misri angeokolewa na Yehova; Angewaua wazaliwa wa kwanza wa kiume na wazaliwa wa kwanza wa kondoo na ng’ombe wao wote. Kwa hivyo, katika vitabu vingi vya unabii kulitabiriwa kwamba Wamisri wangepadibiwa vikali kutokana na agano la Yehova. Hiki ndicho kiwango cha kwanza cha maana cha agano. Yehova Aliwaua wazaliwa wa kwanza wa kiume wa Misri na wazaliwa wa kwanza wa mifugo wao wote, na kuwaacha Waisraeli wote, jambo lililomaanisha kuwa wale wote waliokuwa wa nchi ya Israeli walipendwa na Yehova na wote wangeokolewa; Alidhamiria kufanya kazi ya muda mrefu ndani yao, na Alianzisha agano nao kwa kutumia damu ya mwanakondoo. Tangu wakati ule kuendelea, Yehova Asingewaua Waisraeli na Alisema kuwa daima wangukuwa wateuliwa Wake. Angeianza kazi Yake ya Enzi Nzima ya Sheria Miongoni mwa makabila kumi na mawili ya Israeli, Angeziweka wazi sheria Zake zote kwa Waisraeli, na kuchagua manabii na waamuzi kutoka kati yao, na wangukuwa katikati ya kazi Yake. Yehova Agano nao: Angefanya kazi tu miongoni mwa wateuliwa isipokuwa enzi ibadilike. Agano la Yehova lilikuwa lisilobadilika kwani lilitengenezwa kwa damu, na lilianzishwa na wateuliwa Wake. La muhimu zaidi, Alikuwa Ametewa mawanda na malengo yafaayo ya kazi Yake katika enzi nzima, na kwa hivyo watu walilionga agano kuwa la umuhimu sana. Hiki ndicho kiwango cha pili cha maana ya agano. Isipokuwa kitabu cha Mwanzo, ambacho kilikuwepo kabla ya kuanzishwa kwa agano, vitabu vingine vyote vya Agano la Kale vinaeleza kuhusu kazi ya Mungu miongoni mwa Waisraeli baada ya kuanzishwa kwa agano hili. Bila shaka, yapo maelezo ya hapa na pale ya Watu wa Mataifa, ila kwa ujumla, Agano la Kale linaeleza kuhusu kazi ya Mungu nchini Israeli. Kwa sababu ya Agano kati ya Yehova na Waisraeli, vitabu vilivyoandikwa katika Enzi ya Sheria vinaitwa “Agano la Kale.” Vimepatiwa jina hili kutokana na agano la Yehova na Waisraeli.

Agano Jipya lilipatiwa jina hilo kutokana na damu iliyomwagwa na Yesu msalabani na agano Lake na wale wote waliomwamini. Agano la Yesu lilikuwa hili: Watu hawakuwa na budi kumwamini ili dhambi zao zisamehewe kwa kumwagika kwa damu Yake, na kwa njia hiyo wangeokolewa na kuzaliwa upya kupitia Kwake, na kamwe wasingendelee kuwa wenye dhambi; watu walipaswa kumwamini ili wapokee neema Yake, na hawangeteseka jehanamu

baada ya kufa. Vitabu vyote vilivyoandikwa wakati wa Enzi ya Neema vilizuka baada ya hili agano, na vyote vinaeleza kuhusu kazi na matamshi yaliyomo. Havielezi zaidi ya wokovu wa kusulubishwa kwa Bwana Yesu au hili agano; vyote ni vitabu vilivyoandikwa na wapendwa katika Bwana waliokuwa na tajriba. Kwa hivyo hivi vitabu vilevile vimepatiwa jina kutokana na agano: Vinaitwa Agano Jipya. Haya Maagano mawili yanajumuisha tu Enzi ya Neema na Enzi ya Sheria na hayana uhusiano na enzi ya mwisho. Hivyo basi, Biblia haina msaada mkubwa kwa watu wa leo wa siku za mwisho. Zaidi, hutumika kama marejeleo ya muda mfupi, ila kimsingi haina matumizi ya thamani kubwa. Ila watu wa dini bado wanaienzi kuliko kitu kingine chochote. Hawajui Biblia; wanajua tu jinsi ya kuieleza Biblia na kimsingi hawajui asili yake. Mtazamo wao kuhusu Biblia ni: Kila kitu katika Biblia ni sahihi, haina upungufu au makosa. Kwa sababu kwanza wameshakubali kwamba Biblia iko sahihi, bila makosa, wanaichunguza na kuitathimini kwa shauku kubwa. Hatua ya leo ya kazi haikutabiriwa kwa Biblia. Hakukutajwa kazi ya ushindi katika sehemu za giza zaidi, kwani hii ni kazi mpya zaidi. Kwa sababu enzi ya kazi ni tofauti, hata Yesu Mwenyewe hakufahamu kuwa hatua hii ya kazi ingefanywa katika siku za mwisho—basi, watu wa siku za mwisho wangetathimini vipi kuigundua hii hatua ya kazi katika Biblia?

Wengi wa wale wanaoeleza Biblia wanatumia mitazamo ya kimantiki na hawana usuli wa uhalisia. Wanatumia mantiki tu kuvielewa vitu vingi. Kwa miaka na miaka, hakuna aliyethubutu kuichanganua Biblia, au kusema “hapana” kwa Biblia, kwa sababu kitabu hiki ni kitabu kitakatifu, na watu wanakiabudu kama Mungu. Hili limeendelea kwa maelfu kadhaa ya miaka. Mungu hajashughulishwa na hakuna aliyegundua maelezo wa ndani kuhusu Biblia. Tunasema kwamba kuithamini sana Biblia ni kuabudu miungu, na bado hakuna kati ya hawa waumini anayethubutu kuyaona mambo kwa njia hii, na watakwambia: “Ndugu! Usiseme hivyo, ni vibaya! Wawezaje kumkufuru Mungu?” Baadaye watakuwa na hisia za uchungu: “Lo, Yesu wa huruma, Bwana wa wokovu, nakuomba umsamehe dhambi zake kwa kuwa Wewe ni Bwana Ampendaye mwanadamu, nasi sote tumekosa, tafadhali tuonee huruma kubwa, amina.” Hivi ndivyo jinsi walivyo “wacha Mungu”; ingekuwaje rahisi kwa wao kuukubali ukweli? Msemo wako ambao utawaogopesha sana. Hakuna ambaye angethubutu kufikiri kuwa Biblia ingeweza kupakwa doa na mawazo ya binadamu na dhana za binadamu, na hakuna awezaye kuiona hii dosari. Baadhi ya mambo katika Biblia ni matukio na maarifa ya watu binafsi, baadhi ni kupatiwa nuru ya Roho Mtakatifu, na pia kuna unajisi unaofanywa katika akili na fikra za wanadamu. Mungu hajawahi kuingilia mambo haya lakini kuna kikomo: Mambo haya hayawezi kuzidi fikra ya kawaida ya watu, na yakipita, yatakuwa yakiingilia na kuitatiza kazi ya Mungu. Kile kinachozidi fikra za kawaida za watu ni kazi ya Shetani, kwa kuwa kinatoa watu wajibu wao, ni kazi ya Shetani, na kuelekezwa na Shetani, na katika kipindi hiki Roho Mtakatifu

Hatakuruhusu kutenda mambo kwa njia hiyo. Wakati mwingine ndugu wengine huuliza: “Ni sawa nikitenda mambo kwa namna hii na ile?” Mimi hutazama kimo chao na kusema: “Sawa!” Vilevile kunao watu wengine ambao husema: “Nikitenda namna hii na ile, je, hali yangu ni ya kawaida?” Nami hujibu: “Ndiyo, ni ya kawaida, kawaida haswa!” Wengine husema: “Je, ni sawa nikifanya hivi?” Nami husema: “Hapana!” Wao husema: “Ni kwa nini ni sawa kwake na si sawa kwangu?” Nami husema: “Kwa sababu unachokifanya kinatoka kwa Shetani. Ni mvurugo, na chanzo cha kichocheo chako kinaenda mrama.” Huwepo pia wakati ambapo kazi haisongi kadiri inavyotakiwa na ndugu na dada hawafahamu hili. Wengine huniuliza kama ni sawa kufanya kazi kwa njia fulani, na Nionapo kuwa matendo yao hayatatatiza kazi ya siku za usoni, Mimi husema kwamba ni sawa. Kazi ya Roho Mtakatifu huwapa watu upeo; watu hawalazimiki kufuata mapenzi ya Roho Mtakatifu hadi nukta ya mwisho, kwani watu wana fikra ya kawaida na udhaifu, na wana mahitaji ya kimwili, wana matatizo halisi, na katika bongo zao kuna mawazo ambayo kimsingi hawana njia za kuyadhibiti. Kila Ninachohitaji kutoka kwa wanadamu kina mipaka. Wengine huamini kuwa maneno Yangu yana utata, kwamba Nawaambia kutenda mambo kwa njia yoyote ile—hii ni kwa sababu haufahamu kuwa kuna upeo ufao katika mahitaji Yangu. Ingekuwa unavyodhani—Ningekuwa na mahitaji sawa kwa kila mtu bila kighairi, na kuwahitaji wafikie kimo sawa—basi hili lisingefanyika. Huku ni kuuliza lisilowezekana, na ni kanuni ya kazi ya mwanadamu, si kanuni ya kazi ya Mungu. Kazi ya Mungu huendeshwa kulingana na hali halisi ya wanadamu, na imekitwa katika ubora wao asilia. Hii vilevile ni kanuni ya kueneza injili: Ni lazima uifanye taratibu, na kuruhusu hali asilia kuchukua mkondo wake; wakati tu utakapomwambia mtu ukweli wazi wazi ndipo atakapoelewa, na ni wakati huo tu ndipo ataweza kuiweka Biblia kando. Ikiwa Mungu Asingefanya hatua hii ya kazi, ni nani angeweza kuyavunja desturi? Ni nani angeweza kuifanya kazi mpya? Ni nani angeweza kutafuta njia mpya nje ya Biblia? Kwa sababu dhana za jadi ya watu na maadili ya kijamii ni maudhi, hawana uwezo wa kuviacha hivi vitu wao wenyewe, wala hawana ujasiri wa kufanya hivyo. Hapo ni bila kutaja namna watu wa leo wametekwa na maneno machache yaliyokufa katika Biblia, maneno ambayo yameimiliki mioyo yao. Watakuwaje radhi kuiacha Biblia? Watawezaje kukubali kwa urahisi njia iliyo nje ya Biblia? Hilo haliwezekani pasipo na wewe kuzungumza wazi kuhusu simulizi ya ndani ya Biblia na kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu, ili watu wote washawishiwe kabisa—ambalo ni la haja kubwa. Hii ni kwa sababu kila aliye ndani ya dini anaihesimu Biblia na kuiabudu kama Mungu, vilevile wanajaribu kumfunga Mungu katika mipaka ya Biblia, na ndivyo hutimiza madhumuni yao punde tu wanapomuangika Mungu msalabani kwa mara nyingine.

Kuhusu Biblia (3)

Si kila kitu katika Biblia ni rekodi ya maneno aliyoyasema Mungu. Kimsingi Biblia

inaandika hatua mbili za awali za kazi ya Mungu, ambapo sehemu moja ni rekodi ya utabiri wa kale wa manabii, na sehemu nyingine ni uzoefu na maarifa yaliyoandikwa na watu waliotumiwa na Mungu katika enzi zote. Uzoefu wa kibinadamu umetiwa doa na maoni na maarifa ya kibinadamu, kitu ambacho hakiepukiki. Katika vitabu vingi vya Biblia kuna dhana nyingi za kibinadamu, upendelevu wa binadamu, na ufahamu wa ajabu wa binadamu. Ni kweli, maneno mengi ni matokeo ya kupatiwa nuru na kuangaziwa na Roho Mtakatifu, na ni ufahamu sahihi—lakini haiwezi kusemwa kuwa ni udhihirishaji sahihi kabisa wa ukweli. Maoni yao juu ya vitu fulani si chochote zaidi ya maarifa yaliyotokana na uzoefu binafsi, au kupatiwa nuru na Roho Mtakatifu. Utabiri wa manabii ulikuwa umeagizwa na Mungu binafsi: Unabii wa mifano ya Isaya, Danieli, Ezra, Yereimia, na Ezekieli, ulitoka moja kwa moja kwa Roho Mtakatifu; watu hawa walikuwa ni waonaji maono, walipokea Roho ya Unabii, wote walikuwa ni manabii wa Agano la Kale. Wakati wa Enzi ya Sheria watu hawa, ambao walikuwa wamepokea ufunuo wa Yehova, walizungumza unabii mwingi, ambao ulisemwa na Yehova moja kwa moja. Na kwa nini Yehova alifanya kazi ndani yao? Kwa sababu watu wa Israeli walikuwa ni wateule wa Mungu: Kazi ya manabii ilipaswa kufanyika miongoni mwao, na walikuwa wamefuzu kupokea maono hayo. Kimsingi, wao wenyewe hawakuelewa ufunuo wa Mungu kwao. Roho Mtakatifu Alizungumza maneno hayo kupitia vinywa vyao ili watu wa baadaye waweze kuelewa mambo hayo, na kuona kwamba ni kweli ilikuwa ni kazi ya Roho wa Mungu, ya Roho Mtakatifu, na haikutoka kwa mwanadamu, na kuweza kuwathibitisha kazi ya Roho Mtakatifu. Wakati wa Enzi ya Neema, Yesu Mwenyewe Alifanya kazi hii yote badala yao, na hivyo watu hawakuzungumza tena unabii. Kwa hivyo Yesu alikuwa nabii? Yesu, kimsingi alikuwa ni nabii, lakini pia Alikuwa na uwezo wa kufanya kazi ya mitume—: Aliweza kusema unabii na kuhubiri na kufundisha watu katika nchi yote. Bado kazi Aliyoifanya na utambulisho Aliouwakilisha haukuwa unafanana. Alikuwa kuwakomboa binadamu wote, kumkomboa mwanadamu kutoka dhambini; Alikuwa nabii, na mtume, lakini zaidi ya hapo Alikuwa Kristo. Nabii Anaweza kuzungumza unabii, lakini haiwezi kusemwa kwamba yeye ni Kristo. Wakati huo, Yesu alizungumza unabii mwingi, na hivyo inaweza kusemwa kwamba Alikuwa nabii, lakini haiwezi kusemwa kwamba Alikuwa nabii na hivyo sio Kristo. Hiyo ni kwa sababu Alimwakilisha Mungu Mwenyewe katika kutekeleza hatua ya kazi, na utambulisho Wake ulikuwa tofauti na ule wa Isaya: Alikuwa kukamilisha kazi ya ukombozi, na hivyo Alitoa maisha ya mwanadamu, na Roho wa Mungu Alikuwa Kwake moja kwa moja. Katika kazi Aliyoifanya, hakukuwa na uvuvio wa kutoka kwa Roho wa Mungu au maelekezo kutoka kwa Yehova. Badala yake, Roho alifanya kazi moja kwa moja—kitu ambacho kinatosha kuthibitisha kwamba Yesu Hakuwa sawa na nabii. Kazi Aliyoifanya ilikuwa ni kazi ya ukombozi, kazi iliyoifuatia ilikuwa ni kuzungumza unabii. Alikuwa ni nabii, mtume, na zaidi ya hapo Alikuwa ni Mkombozi. Wakati huo, watabiri, wangeweza tu kuzungumza unabii, na walikuwa hawana uwezo wa kumwakilisha Roho wa

Mungu katika kufanya kazi nyingine yoyote. Kwa sababu Yesu alifanya kazi kubwa ambayo haijawahi kufanywa na binadamu, na Alifanya kazi ya kumkomboa mwanadamu, kwa hiyo Alikuwa tofauti na manabii wengine kama Isaya. Kwamba watu wengine hawakubali mkondo wa leo ni kwa sababu hii imetengeneza kizuizi kwao. Wanasema: “Katika Agano Jipya manabii wengi pia walisema maneno mengi—sasa, kwa nini hawakuwa Mungu katika mwili? Mungu wa leo Anazungumza maneno—je, hii inatosha kuthibitisha kuwa Yeye ni Mungu mwenye mwili? Huipatii Biblia umuhimu mkubwa, wala huichunguzi, sasa una msingi gani wa kusema kwamba Yeye ni Mungu aliyepata mwili? Unasema kwamba wameongozwa na Roho Mtakatifu, na unaamini kwamba hatua hii ya kazi ni kazi ambayo imefanywa na Mungu Mwenyewe—lakini msingi wako kwa hili ni nini?” Umetilia mkazo katika maneno ya Mungu leo, inaonekana kana kwamba umeikana Biblia, na kuiweka katika upande mmoja.” Na hivyo wanasema kwamba unaamini uzushi, na imani mbalimbali.

Ikiwa unatamani kuwa na ushuhuda kwa kazi ya Mungu wakati wa siku za mwisho, basi unapaswa kuelewa kisa cha ndani cha Biblia, muundo wa Biblia, na hulka ya Biblia. Leo, watu wanaamini kwamba Biblia ni Mungu, na kwamba Mungu ni Biblia. Na hivyo pia, wanaamini kwamba maneno yote ya Biblia ni maneno pekee ambayo Mungu alizungumza, na kwamba yote yalizungumzwa na Mungu. Wale wanaomwamini Mungu hata wanafikia hatua ya kufikiri kwamba ingawa vitabu vyote sitini na sita vya Agano la Kale na Agano Jipya viliandikwa na watu, vyote viliandikwa kwa uvuvio wa Mungu, na ni rekodi ya matamshi ya Roho Mtakatifu. Huu ni ufahamu wenye makosa wa mwanadamu, na hauafikiani kabisa na kweli. Kimsingi, mbali na vitabu vya unabii, sehemu kubwa ya Agano la Kale ni rekodi ya kihistoria. Baadhi ya nyaraka za Agano Jipya zinatokana na uzoefu wa watu, na baadhi zinatokana na kupatiwa nuru na Roho Mtakatifu; nyaraka za Paulo, kwa mfano, zilitokana na kazi ya mwanadamu, zote zilitokana na kupatiwa nuru na Roho Mtakatifu, na ziliandikwa kwa ajili ya makanisa, yalikuwa ni maneno ya kushawishi na kutia moyo kwa kaka na dada wa makanisa. Hayakuwa maneno yaliyozungumzwa na Roho Mtakatifu—Paulo asingeweza kuzungumza kwa niaba ya Roho Mtakatifu, na wala hakuwa nabii, sembuse kuona maono ambayo Yohana aliona. Nyaraka zake ziliandikwa kwa ajili ya makanisa ya Efeso, Filadefia, Galatia, na makanisa mengineyo. Na hivyo, nyaraka za Paulo za Agano Jipya ni nyaraka ambazo Paulo aliandika kwa ajili ya makanisa, na sio uvuvio wa Roho Mtakatifu, wala sio matamshi ya moja kwa moja ya Roho Mtakatifu. Ni maneno tu ya kushawishi, faraja, na kutia moyo ambayo aliyaandika kwa ajili ya makanisa wakati wa kazi yake. Na hivyo pia, ni rekodi zaidi ya kazi na muda ya Paulo. Ziliandikwa kwa ajili ya kaka na dada wote katika Bwana, na zilikuwa ni kwa ajili ya kuwafanya kaka na dada wa makani yote ya wakati huo kufuata ushauri wake na kudumu siku zote katika njia zote za Bwana Yesu. Kwa namna yoyote ile Paulo hakusema kuwa, iwe ni kwa makanisa ya

wakati huo au makanisa ya wakati ujao, yote yanapaswa kula na kunywa vitu alivyoandika, wala hakusema kwamba maneno yake yote yalitoka kwa Mungu. Kulingana na mazingira ya kanisa wakati huo, aliwasiliana tu na kaka na dada, na aliwashawishi, na akawaimarisha imani kwao; na aliwahubiria na kuwakumbusha watu na kuwashawishi. Maneno yake yalijikita katika mzigo wake mwenyewe, na aliwasaidia watu kupitia maneno haya. Alifanya kazi ya mitume wa kanisa wa wakati huo, alikuwa mfanyakazi ambaye alitumiwa na Bwana Yesu, na kwa hivyo lazima achukue jukumu kwa ajili ya makanisa, na lazima afanye kazi ya makanisa, alipaswa kujifunza kuhusu hali za ndugu—na kwa sababu hii, aliandika nyaraka kwa kaka na dada wote katika Bwana. Yote aliyoyasema ambayo yaliyokuwa ni ya kuadilisha na mazuri kwa watu yalikuwa sahihi, lakini hayakuwa yanawakilisha matamshi ya Roho Mtakatifu, na hayakuweza kumwakilisha Mungu. Ni uelewa mbaya kupita kiasi, na makufuru makubwa sana kwa watu kuchukulia rekodi za uzoefu wa mwanadamu na nyaraka za mwanadamu kama maneno yaliyozungumzwa na Roho Mtakatifu kwa makanisa! Hiyo ni kweli kabisa tunapokuja katika nyaraka ambazo Paulo aliziandika kwa ajili ya makanisa, kwani nyaraka zake ziliandikwa kwa ajili ya kaka na dada kulingana na mazingira na hali ya kila kanisa kwa wakati huo, na yalikuwa ni kwa ajili ya kuwashawishi kaka na dada katika Bwana, ili waweze kupokea neema ya Bwana Yesu. Nyaraka zake zilikuwa ni kwa ajili ya kuwaamsha kaka na dada wa wakati huo. Inaweza kusemwa kuwa huu ulikuwa ni mzigo wake mwenyewe, na pia ulikuwa ni mzigo aliopewa na Roho Mtakatifu; hata hivyo, alikuwa ni mtume aliyeyaongoza makanisa ya wakati huo, ambaye aliandika nyaraka kwa ajili ya makanisa na kuwashawishi, huo ulikuwa wajibu wake. Utambulisho wake ulikuwa tu ni mtume anayefanya kazi, na alikuwa ni mtume tu aliyetumwa na Mungu; hakuwa mtabiri, wala mtoa unabii. Kwake, kazi yake mwenyewe na maisha ya kaka na dada yalikuwa na umuhimu mkubwa sana. Hivyo, asingeweza kuzungumza kwa niaba ya Roho Mtakatifu. Maneno yake hayakuwa maneno ya Roho Mtakatifu, wala yasingesemwa kuwa ni maneno ya Mungu, maana Paulo hakuwa chochote zaidi ya kiumbe wa Mungu, na hakika hakuwa Mungu aliyepata mwili. Utambulisho wake haukuwa sawa na ule wa Yesu. Maneno ya Yesu yalikuwa ni maneno ya Roho Mtakatifu, yalikuwa ni maneno ya Mungu, maana utambulisho wake ulikuwa ule wa Kristo—Mwana wa Mungu. Inawezekanaje Awe sawa na Paulo? Ikiwa watu wanaona nyaraka au maneno kama ya Paulo kama matamshi ya Roho Mtakatifu, na kuwaabudu kama Mungu, basi inaweza kusemwa tu kuwa ni watu wasiochagua kwa busara. Tukisema kwa ukali zaidi, haya sio makufuru? Inawezekanaje mwanadamu azungumze kwa niaba ya Mungu? Na inawezekanaje watu wapigie magoti rekodi za nyaraka zake na maneno aliyoyazungumza kana kwamba yalikuwa ni kitabu kitakatifu, au kitabu cha mbinguni? Je, inawezekana maneno ya Mungu kutamkwa kwa kawaida na mwanadamu? Inawezekanaje mwanadamu azungumze kwa niaba ya Mungu? Na hivyo, unasemaje—kwamba nyaraka alizoandika kwa ajili ya makanisa haziwezi kutiwa doa na mawazo yake mwenyewe?

Inawezekanaje zisitiwe doa na mawazo ya kibinadamu? Aliandika nyaraka kwa makanisa kulingana na uzoefu wake binafsi, na maarifa yake binafsi. Kwa mfano, Paulo aliandika waraka kwa kanisa la Wagalatia ambao ulikuwa na maoni fulani, na Petro aliandika waraka mwingine, ambao ulikuwa na mtazamo mwingine. Ni upi kati ya hizo ulitoka kwa Roho Mtakatifu? Hakuna anayeweza kutoa jibu, hakika. Hivyo inaweza kusemwa tu kwamba wote wanawiwa na mzigo kwa makanisa, lakini barua zao zinawakilisha kimo chao, zinawakilisha vile wanavyowapatia na kuwasaidia kaka na dada, na vile wanavyowiwa na makanisa, na zinawakilisha tu kazi ya binadamu; hayakuwa ya Roho Mtakatifu kabisa. Ikiwa unasema kwamba nyaraka zake ni maneno ya Roho Mtakatifu, basi wewe ni mpumbavu, na unafanya makufuru! Nyaraka za Paulo na nyaraka nyingine za Agano Jipya ni sawa na kumbukumbu za viongozi mashuhuri wa kiroho wa hivi karibuni. Zipo sawa na vitabu vya Watchman Nee au uzoefu wa Lawrence, na kadhalika. Ni vile tu vitabu vya viongozi mashuhuri wa kiroho wa hivi karibuni havijajumuishwa katika Agano Jipya, lakini hulka ya watu hawa ni sawa: Kulikuwa na watu ambao walitumiwa na Roho Mtakatifu wakati fulani, na hawakuweza kumwakilisha Mungu moja kwa moja.

Injili ya Mathayo ya Agano Jipya inaandika ukoo wa Yesu. Mwanzoni, inasema kwamba Yesu alikuwa mzao wa Abrahamu na wa Daudi, na mwana wa Yusufu; sehemu inayofuata inasema kwamba Yesu alizaliwa kwa njia ya Roho Mtakatifu, na kuzaliwa na bikira—kitu kinachomaanisha kwamba Hakuwa mwana wa Yusufu au mzao wa Abrahamu na wa Daudi. Hata hivyo, orodha ya ukoo inasisitiza kumhusisha Yesu na Yusufu. Sehemu inayofuata, orodha ya ukoo inaanza kurekodi mchakato ambao kwa huo Yesu alizaliwa. Inasema mimba ya Yesu ilitungwa kwa njia ya Roho Mtakatifu, kwamba Alizaliwa na bikira, na sio mwana wa Yusufu. Lakini katika orodha ya ukoo imeandikwa waziwazi kwamba Yesu alikuwa mwana wa Yusufu, na kwa kuwa orodha ya ukoo iliandikwa kwa ajili ya Yesu, inaandika vizazi arobaini na mbili. Inapokwenda katika ukoo wa Yusufu, inasema kwa haraka kwamba Yusufu alikuwa mume wa Mariamu, haya ni maneno kwa ajili ya kuthibitisha kwamba Yesu alikuwa mzao wa Abrahamu. Je, huu si mkanganyiko? Orodha hii ya ukoo inaonyesha waziwazi chimbuko la Yusufu, ni wazi kwamba hii ni orodha ya ukoo wa Yusufu, lakini Mathayo anasisitiza kwamba ni orodha ya ukoo wa Yesu. Je, hii haipingi ukweli kwamba Yesu alizaliwa kwa njia ya Roho Mtakatifu? Hivyo, orodha ya ukoo iliyoandikwa na Mathayo sio mawazo ya kibinadamu? Hii ni dhihaka! Kwa namna hii, unaweza kujua kwamba kitabu hiki sio chote kimetoka kwa Roho Mtakatifu. Pengine, kuna baadhi ya watu wanaodhani kwamba Mungu lazima atakuwa na orodha ya ukoo duniani, na matokeo yake ni kwamba wanampachika Yesu kama kizazi cha arobaini na viwili cha Abrahamu. Hii ni dhihaka kabisa! Baada ya kuja duniani, Mungu angewezaje kuwa na orodha ya ukoo? Ikiwa unasema kwamba Mungu ana ukoo, je, humweki katika madaraja sawa miongoni mwa viumbe wa Mungu? Maana Mungu si wa ulimwengu, Yeye ni Bwana wa uumbaji, na

ingawa yeye ni wa mwili, hana asili sawa na mwanadamu. Unawezaje kumweka Mungu katika daraja sawa na viumbe wa Mungu? Abrahamu hawezi kumwakilisha Mungu; alikuwa ni mhusika wa kazi ya Yehova wakati huo, alikuwa ni mtumishi mwaminifu tu aliyethibitishwa na Yehova, na alikuwa mmoja wa watu wa Israeli. Inawezekanaje awe babu wa Yesu?

Ni nani aliandika orodha ya ukoo wa Yesu? Ni Yesu Mwenyewe ndiye aliyeandika? Je, ni Yesu Mwenyewe ndiye Alisema, “Andika orodha Yangu ya ukoo”? Iliandikwa na Mathayo baada ya Yesu kuangikwa msalabani. Wakati huo, Yesu alikuwa amefanya kazi kubwa ambayo ilikuwa haifahamiki kwa mitume, na Hakutoa maelezo yoyote. Baada ya Yeye kuondoka, mitume walianza kuhubiri na kufanya kazi kila mahali, na kwa ajili ya hatua hiyo ya kazi, walianza kuandika nyaraka na vitabu vya injili. Vitabu vya injili ya Agano Jipya vilirekodiwa miaka ishirini hadi thelathini baada ya Yesu kusulubiwa msalabani. Kabla ya hapo, watu wa Israeli walisoma tu Agano la Kale. Hiyo ni sawa na kusema, mwanzoni mwa Enzi ya Neema watu walisoma Agano la Kale. Agano Jipya lilionekana tu wakati wa Enzi ya Neema. Agano Jipya halikuwepo wakati wa kazi ya Yesu; watu waliandika kazi Yake baada ya kuwa amefufuka na kupaa mbinguni. Baada ya hapo kulikuwa na Injili Nne, katika nyongeza hiyo pia kulikuwa na nyaraka za Paulo na Petro, na vile vile kitabu cha Ufunuo. Ni baada tu ya zaidi ya miaka mia tatu baada ya Yesu kupaa mbinguni, wakati vizazi vilivyofuata viliweka pamoja rekodi zao, ndipo kulikuwa na Agano Jipya. Ni baada tu ya kazi hii kukamilika ndipo kukapatikana Agano Jipya; halikuwepo hapo kabla. Mungu alikuwa amefanya kazi yote hiyo, mtume Paulo alifanya kazi yote hiyo, na baadaye nyaraka za Paulo na Petro ziliunganishwa, na njozi kuu zaidi iliyorekodiwa na Yohana katika kisiwa cha Patmo iliwekwa mwishoni, maana ilikuwa inatoa unabii wa kazi ya siku za mwisho. Hii yote ilikuwa ni mipango ya vizazi vilivyofuata na ni tofauti na matamshi ya leo. Kile kilichorekodiwa leo ni kulingana na hatua za kazi ya Mungu; kile ambacho watu wanashughulika nacho leo ni kazi ambayo imefanywa na Mungu Mwenyewe, na maneno yaliyotamkwa na Mungu Mwenyewe. Wewe—mwanadamu—hupaswi kuingilia; maneno, ambayo yanatoka moja kwa moja kwa Roho Mtakatifu, yamepangwa hatua kwa hatua, na ni tofauti na mpangilio wa rekodi za wanadamu. Inaweza kusemwa kuwa, kile walichorekodi kilikuwa ni kulingana na kiwango chao cha elimu na tabia. Kile walichokirekodi kilikuwa ni uzoefu wa wanadamu, na kila mmoja alikuwa na namna yake ya kurekodi na kuelewa, na kila rekodi ilikuwa tofauti. Hivyo, ikiwa unaiabudu Biblia kama Mungu wewe ni mjinga na mpumbavu wa kutupwa! Kwa nini usitafute kazi ya Mungu wa leo? Ni kazi ya Mungu tu ndiyo inayoweza kumwokoia mwanadamu. Biblia haiwezi kuwaokoa wanadamu, wanaweza kuisoma kwa maelfu kadhaa ya miaka na bado hakutakuwa na mabadiliko hata kidogo ndani yao, na kama unaiabudu Biblia hutaweza kupata kazi ya Roho Mtakatifu. Hatua mbili za kazi ya Mungu katika Israeli zote zimerekodiwa katika Biblia, na hivyo miongoni mwa rekodi hizi majina yote

ni ya Israeli, na matukio yote ni ya Israeli; na hata jina “Yesu” ni jina la Kiisraeli. Ikiwa unaendelea kusoma Biblia leo, huoni unafungamanishwa kwa maagano? Yale yaliyorekodiwa katika Agano Jipya la Biblia ni masuala ya Yudea. Matini ya awali yalikuwa katika Kiyunani na Kiebrania, na maneno ya Yesu, na jina ambalo kwalo Aliitwa wakati huo ambapo yote yalikuwa katika lugha ya mwanadamu. Aliposulubiwa msalabani, Yesu Alisema: “Eloi, Eloi, lama sabakthani” Je, hiki sio Kiebrania? Hii tu ni kwa sababu Yesu alipata mwili Yudea, lakini haithibitishi kwamba Mungu ni Myahudi. Leo, Mungu amefanyika mwili China, na hivyo kila kitu Anachokisema bila shaka ni katika lugha ya Kichina. Lakini hakiwezi kulinganishwa na Kichina kilichotafsiriwa kutoka katika Biblia, maana chanzo cha maneno haya ni tofauti. Moja inatoka kwa Kiebrania kilichorekodiwa na watu, na moja inatoka katika matamshi ya moja kwa moja ya Roho. Kunawezaje kutokuwa na tofauti hata kidogo?

Kuhusu Biblia (4)

Watu wengi wanaamini kwamba kuelewa na kuwa na uwezo wa kufasiri Biblia ni sawa na kutafuta njia ya kweli—lakini, kimsingi, je, vitu ni rahisi sana? Hakuna anayejua uhalisia wa Biblia: kwamba si kitu chochote zaidi ya rekodi ya kihistoria ya kazi ya Mungu, na agano la hatua mbili zilizopita za kazi ya Mungu, na haikupatii ufahamu wa malengo ya kazi ya Mungu. Kila mtu ambaye amesoma Biblia anajua kwamba inarekodi hatua mbili za kazi ya Mungu wakati wa Enzi ya Sheria na Enzi ya Neema. Agano la Kale linaandika historia ya Israeli na kazi ya Yehova kuanzia wakati wa uumbaji hadi mwisho wa Enzi ya Sheria. Agano Jipya linarekodi kazi ya Yesu duniani, ambayo ipo katika Injili Nne, vilevile kazi ya Paulo; je, sio rekodi za kihistoria? Kuleta mambo ya zamani leo kunayafanya yawe historia, haijalishi yana ukweli kiasi gani, bado ni historia—na historia haiwezi kushughulikia masuala ya leo. Maana Mungu haangalii historia! Na hivyo, kama unaelewa tu Biblia, na huelewi chochote kuhusu kazi ambayo Mungu anakusudia kufanya leo, na kama unamwamini Mungu, na hutafuti kazi ya Roho Mtakatifu, basi hujui inamaanisha nini kumtafuta Mungu. Ikiwa unasoma Biblia kwa lengo la kujifunza historia ya Israeli, kutafiti historia ya uumbaji wa Mungu wa mbingu na dunia, basi humwamini Mungu. Lakini leo, kwa kuwa unamwamini Mungu, na kutafuta uzima, kwa kuwa unatafuta maarifa juu ya Mungu, na hutafuti nyaraka na mafundisho mfu, au ufahamu wa historia, unapaswa kutafuta mapenzi ya Mungu ya leo, na unapaswa kutafuta uongozi wa kazi ya Roho Mtakatifu. Kama ungekuwa mwanaakiolojia ungeweza kusoma Biblia—lakini wewe sio mwanaakiolojia, wewe ni mmoja wa wale wanaomwamini Mungu, na utakuwa bora zaidi ukitafta mapenzi ya Mungu ya leo. Kwa kusoma Biblia, angalau utakuwa umeelewa sehemu ndogo ya historia ya Israeli, utajifunza kuhusu maisha ya Abrahamu, Daudi, na Musa, utajua kuhusu namna walivyomheshimu sana Yehova, namna ambavyo Yehova aliwachoma wale waliompinga, na jinsi alivyozungumza na watu wa enzi hiyo. Utaelewa tu kuhusu kazi ya Mungu

katika wakati uliopita. Rekodi za Biblia zinahusiana na jinsi ambavyo watu wa awali wa Israeli walivyomheshimu sana Mungu na kuishi chini ya uongozi wa Yehova. Kwa sababu Waisraeli walikuwa ni wateuliwa wa Mungu, katika Agano la Kale unaweza kuona utii wote wa watu wa Israeli kwa Yehova, jinsi ambavyo wale wote waliomtii Yehova walivyokuwa wanaangaliwa na kubarikiwa Naye, unaweza kujifunza kwamba Mungu alipofanya kazi katika Israeli alikuwa mwingi wa rehema na mapenzi, vilevile alikuwa na moto uteketezao, na kwamba Waisraeli wote, kuanzia watu wa chini hadi wakubwa, walimheshimu sana Yehova, na hivyo nchi yote ilibarikiwa na Mungu. Hiyo ni historia ya Israeli iliyorekodiwa katika Agano la Kale.

Biblia ni rekodi ya kihistoria ya kazi ya Mungu katika Israeli, na inaandika utabiri mwingi wa manabii wa kale vilevile baadhi ya matamshi ya Yehova katika kazi Yake wakati huo. Hivyo, watu wote wanakitazama kitabu hiki kama kitakatifu (maana Mungu ni mtakatifu na mkuu). Kimsingi, hii yote ni matokeo ya uchaji wao kwa Yehova na vile walivyokuwa wanampenda Mungu. Watu wanarejelea kitabu hiki kwa namna hii kwa sababu tu viumbe wa Mungu wacha Mungu na wanampenda Muumba wao sana, na hata kuna wale ambao wanakiita kitabu hiki kitabu cha mbinguni. Kimsingi, ni rekodi tu za kibinadamu. Hakikupewa jina na Yehova Mwenyewe, wala Yehova Mwenyewe hakuongoza utengenezaji wake. Kwa maneno mengine, mwandishi wa kitabu hiki sio Mungu, bali ni wanadamu. Biblia Takatifu ni jina la heshima tu lililotolewa na mwanadamu. Jina hili halikuamuliwa na Yehova na Yesu baada ya Wao kujadiliana; si chochote zaidi ya mawazo ya kibinadamu. Maana kitabu hiki hakikuandikwa na Yehova, wala kuandikwa na Yesu. Badala yake, ni maelezo yaliyotolewa na manabii wengi wa kale, mitume na waonaji maono, ambayo baadaye yalipangiliwa na vizazi vilivyofuata na kuwa kitabu cha maandiko ya kale, ambayo kwa watu, yanaonekana kuwa matakatifu, kitabu ambacho wanaamini kimejumuisha siri nyingi ambazo hazieleweki na za kina ambazo zinasubiri kufunguliwa na vizazi vijavyo. Kwa namna hiyo, watu hata wanaamini kwamba kitabu hiki ni kitabu cha mbinguni. Ukijumlisha Injili Nne na Kitabu cha Ufunuo, mtazamo wa watu kuhusu kitabu hicho ni tofauti kabisa na vitabu vingine, na hivyo hakuna mtu anayethubutu kukichambua hiki “kitabu cha mbinguni” kwa sababu ni “kitakatifu” sana.

Kwa nini, mara tu baada ya watu kusoma Biblia wanakuwa na uwezo wa kupata njia sahihi ya kukiweka katika matendo? Kwa nini wanakuwa na uwezo wa kupata mengi ambayo yalikuwa hayafahamiki kwao? Leo, Ninaichambua Biblia kwa namna hii na haimaanishi kwamba Naichukia, au kukana thamani yake kwa ajili ya marejeleo. Ninakuelezea na kukufafanulia thamani ya asili na chanzo cha Biblia ili uweze kuondoka katika giza. Maana watu wana mitazamo mingi kuhusu Biblia, na mingi yao ina makosa; kusoma Biblia kwa namna hii sio tu kunawazuia kupata kile wanachopaswa kupata, lakini, muhimu zaidi, kunazuia kazi Niliyokusudia kufanya. Inaingilia kati kazi ya siku zijazo kwa kiasi kikubwa, na inatoa hasara tu,

na wala sio faida. Hivyo, Ninachokufundisha ni hulka tu na kisa cha ndani cha Biblia. Sikwambii kwamba usisome Biblia, au uzunguke ukitangaza kwamba haina thamani kabisa, bali kwamba uweze kuwa na maarifa na mtazamo sahihi juu ya Biblia. Usiegemee upande mmoja sana! Ingawa Biblia ni kitabu cha historia kilichoandikwa na wanadamu, pia kinaandika kanuni nyingi ambazo kwazo watakatifu wa zamani na manabii walimhudumia Mungu, vilevile uzoefu wa hivi karibuni wa mitume katika kumhudumia Mungu—yote haya yalishuhudiwa na kujulikana kwa watu hawa, na inaweza kutumika kama rejeleo kwa ajili ya watu wa enzi hii katika kutafuta njia ya kweli. Hivyo, katika kusoma Biblia watu wanaweza pia kupata njia nyingi za maisha ambazo haziwezi kupatikana katika vitabu vingine. Njia hizi ni njia za maisha ya kazi ya Roho Mtakatifu ambazo manabii na mitume walizipitia katika enzi iliyopita, na maneno mengi ni ya thamani, na yanaweza kutoa kile ambacho watu wanataka. Hivyo, watu wote wanapenda kusoma Biblia. Kwa sababu kuna mambo mengi sana yaliyofichwa katika Biblia, mitazamo ya watu juu ya Biblia ni tofauti na mitazamo yao juu ya maandiko ya viongozi wa kiroho mashuhuri. Biblia ni rekodi na mkusanyiko wa uzoefu na maarifa ya watu ambao walimhudumia Yehova na Yesu katika enzi ya kale na mpya, na pia vizazi vya baadaye vimeweza kupata nuru, mwanga mkubwa na njia za kuweza kutembea kwazo. Sababu ya Biblia kuwa na hadhi ya juu kuliko maandiko ya kiongozi yeyote mkubwa wa kiroho ni kwa sababu maandiko yao yote yanatoka katika Biblia, uzoefu wao wote unatokana na Biblia, na wote wanaelezea Biblia. Na hivyo, ingawa watu wanaweza wakafaidika na vitabu kutoka kwa kiongozi yeyote wa kiroho mashuhuri, bado wanaibabudu Biblia, maana kwao, inaonekana ni ya juu sana na ya kina sana! Ingawa Biblia inaleta pamoja baadhi ya vitabu vya maneno ya uzima, kama vile nyaraka za Paulo na nyaraka za Petro, na ingawa watu wanaweza kusaidiwa na vitabu hivi, vitabu hivi bado vimepitwa na wakati, bado ni vitabu vya enzi ya kale, na haijalishi ni vizuri kiasi gani, vinafaa tu kwa ajili ya kipindi kimoja, na wala sio vya milele. Maana kazi ya Mungu siku zote inaendelea, na haiwezi kusimama tu katika kipindi cha Paulo na Petro, au siku zote ibaki katika Enzi ya Neema, enzi ambayo Yesu alisulubiwa. Na hivyo, vitabu hivi vinafaa tu katika Enzi ya Neema, na wala sio kwa ajili ya Enzi ya Ufalme wa siku za mwisho. Vinaweza tu kuwa na manufaa kwa waumini wa Enzi ya Neema, na sio kwa watakatifu wa Enzi ya Ufalme, na haijalishi ni vizuri kiasi gani, bado havifai kwa kipindi hiki. Ni sawa na kazi ya Yehova ya uumbaji au kazi Yake katika Israeli: Haijalishi kazi hii ilikuwa kubwa kiasi gani, bado imepitwa na wakati, na muda utaendelea kuja wakati umekwishapita. Kazi ya Mungu pia ni ile ile: Ni nzuri, lakini muda utafika ambapo itakoma; siku zote haitaendelea kubaki katikati ya kazi ya uumbaji, wala katikati ya kazi ile ya msalaba. Haijalishi kazi ya msalaba inashawishi kiasi gani, haijalishi ilikuwa ya ufanisi kiasi gani katika kumshinda Shetani, hata hivyo, kazi bado ni kazi, na enzi, hata hivyo bado ni enzi; kazi siku zote haiwezi kubaki katika msingi ule ule, wala nyakati haziwezi kukosa kubadilika, kwa sababu kulikuwa na uumbaji na lazima kuwepo na siku za mwisho. Hii haiepukiki! Hivyo,

leo maneno ya uzima katika Agano Jipya—nyaraka za mitume, na Injili Nne—vimekuwa vitabu vya kihistoria, vimekuwa vitabu vya kale, na inawezekanaje vitabu vya kale kuwapeleka watu katika enzi mpya? Haijalishi ni kiasi gani vitabu hivi vinaweza kuwapatia watu uzima, haijalishi vina uwezo kiasi gani katika kuwaongoza watu kwenye msalaba, ndio kwamba havijapitwa na wakati? Havijaondokewa na thamani? Hivyo, Ninasema hupaswi kuviamini vitabu hivi bila kufikiri. Ni vya zamani sana, haviwezi kukupeleka katika kazi mpya, vinaweza kukulemea tu. Sio tu haviwezi kukuleta katika kazi mpya, na katika kuingia kupya, bali vinakupeleka katika makanisa ya dini ya kale na kama ni hivyo, havirudishi nyuma imani yako kwa Mungu?

Kile Biblia inaandika ni kazi ya Mungu huko Israeli, pamoja na baadhi ya kile kilichofanywa na watu wateule wa Israeli. Licha ya ukweli kwamba kulikuwa na uchaguzi kadhaa za sehemu zinazopaswa kujumuishwa au kuachwa, hata ingawa Roho Mtakatifu hakukubali, bado Hakuweka lawama yoyote. Biblia ni historia ya Israeli tu, ambayo pia ni historia ya kazi ya Mungu. Watu, masuala, na mambo inayoyarekodi yote yalikuwa ya kweli, na hakuna kitu kuhusu hayo kilikuwa na maana fiche—mbali na unabii wa Isaya, Danieli, na manabii wengine, au kitabu cha Yohana cha maono. Watu wa awali wa Israeli walikuwa wenye maarifa na watu wenye utamaduni wa hali ya juu, na maarifa yao ya kale na utamaduni ulikuwa wa kiwango cha juu, na hivyo kile walichoandika kilikuwa cha kiwango cha juu kuliko watu wa leo. Na hivyo, walikuwa na uwezo mkubwa wa kuandika vitabu hivi, kwa hiyo sio ajabu, maana Yehova alikuwa amefanya kazi kubwa sana miongoni mwao, na walikuwa wameona mengi sana. Daudi alitazama matendo ya Yehova kwa macho yake mwenyewe, yeye mwenyewe aliyashuhudia, na aliona ishara na maajabu mengi sana, na hivyo aliandika zaburi zote hizo kutukuza matendo ya Yehova. Waliweza kuandika vitabu hivi katika mazingira fulani, sio kwa sababu walikuwa watakatifu. Walimtukuza Yehova kwa sababu walikuwa wamemwona. Kama hamjawahi kuona kitu chochote kwa Yehova, na hamjui juu ya uwepo Wake, mnawezaje kumtukuza? Ikiwa hamjawahi kumwona Yehova, basi hamtajua jinsi ya kumtukuza, wala kumwabudu, wala kuweza kuandika nyimbo za kumsifu, na hata kama mtaombwa kuvumbua baadhi ya matendo ya Yehova hamtakuwa na uwezo wa kufanya hivyo. Kwamba, leo, mnaweza kumtukuza Mungu na kumpenda Mungu pia ni kwa sababu mmemwona, na pia mmepitia kazi Yake—na ikiwa tabia yenu inaboreka, ninyi pia hamtakuwa na uwezo wa kuandika mashairi ya kumsifu Mungu kama Daudi?

Ili kuelewa Biblia, kuelewa historia, bali sio kuelewa kile ambacho Roho Mtakatifu anafanya leo—hayo ni makosa! Umeafanya vizuri sana katika kujifunza historia, umefanya kazi nzuri sana, lakini huelewi chochote juu ya kazi Anayofanya Roho Mtakatifu leo. Je, huu si upumbavu? Watu wengine wanakuuliza: “Mungu anafanya nini leo? Ni kitu gani unapaswa kuingia kwacho leo? Maisha yako yanakwendaje? Je, unaelewa mapenzi ya Mungu?” Hutakuwa

na majibu ya kile wanachouliza—sasa unajua nini kwani? Utasema: Ninajua tu kwamba ninapaswa kupuuzia mambo ya mwili na kujitambua. Halafu wakiuliza tena “Ni kitu gani kingine ambacho unakielewa?” Utasema unajua pia kutii mipangilio yote ya Mungu, na kujua kidogo kuhusu historia ya Biblia, basi. Hicho tu ndicho umepata kwa kumwamini Mungu miaka yote hii? Ikiwa hayo tu ndiyo unayoyaelewa, basi unapungukiwa mengi sana. Hivyo, kimo chenu sasa kimsingi hakiwezi kufanikisha yale ambayo Ninayataka kutoka kwenu, na ukweli mnaoufahamu ni mdogo sana, pamoja na uwezo wenu wa kutofautisha—ni sawa na kusema, imani yenu ni ya juujuu sana! Mnapaswa kuwa na kweli zaidi ya hapo, mnahitaji maarifa zaidi, mnapaswa kutazama zaidi, na baada ya hapo tu ndipo mtakuwa mnaweza kusambaza injili, maana hiki ndicho mnapaswa kukipata!

Utendaji (1)

Hapo awali, kulikuwa na mikengeuko mingi na hata mambo ya kipuuzi katika namna ambazo watu walipata uzoefu. Hawakuelewa kabisa viwango vya mahitaji ya Mungu, kwa hiyo kulikuwa na sehemu nyingi ambapo uzoefu wa watu ulienda kombo. Kile Mungu anachohitaji kutoka kwa mwanadamu ni kwa yeye kuweza kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida. Kwa mfano, ni sawa kwa watu kufuata desturi za kawaida kuhusia na chakula na mavazi kuvaa suti na tai, kujifunza kiasi kuhusu sanaa ya kisasa, na wanaweza kufurahia sanaa, utamaduni na burudani katika muda wao wa ziada. Wanaweza kupiga picha kadhaa za kukumbukwa, wanaweza kusoma na kupata maarifa fulani yenye maana, na kuwa na mazingira mazuri kiasi ya kuishi. Haya ndiyo mambo yote ambayo yanastahili maisha ya ubinadamu wa kawaida, ilhali watu wanayaona kama mambo yanayochukiwa na Mungu na wao wanajizua wasiyafanye. Utendaji wao unahusu kufuata kanuni chache tu, jambo ambalo husababisha maisha yasiyo machangamfu na yasiyo na maana yoyote hata kidogo. Kwa kweli, Mungu hajawahi kuhitaji watu watende mambo kwa namna hii. Watu wote wanataka kukatiza tabia zao wenyewe, wakiomba bila kukoma rohoni mwao ili wawe karibu na Mungu, mawazo yao yakifikiria daima kile Mungu anachokusudia, macho yao yakiangalia huku na kule mara kwa mara, wakihofu sana kwamba uhusiano wao kwa Mungu utaharibika kwa namna fulani. Haya yote ni maoni ambayo watu wameibua wao wenyewe; ni sheria ambazo zimewekwa na watu kwa ajili yao wenyewe. Ikiwa hujui kiini na asili yako mwenyewe na huelewi kile kiwango ambacho utendaji wako mwenyewe unaweza kufikia, basi hutakuwa na namna yoyote ya kuwa na hakika ni viwango vipi hasa ambavyo Mungu anahitaji kutoka kwa mwanadamu, na wala hutakuwa na njia mwafaka ya utendaji. Kwa kuwa huwezi kuelewa ni nini hasa ambacho Mungu anahitaji kutoka kwa mwanadamu, akili yako inavurugika daima, unatafakari ukichanganua nia za Mungu na kubabaika ukitaifuta namna fulani ya kuguzwa na kupatiwa nuru na Roho Mtakatifu. Hivyo, unakuza njia fulani za kutenda ambazo unaamini kuwa zinafaa. Huna habari hata kidogo kuhusu

kile hasa Mungu anachohitaji kutoka kwa mwanadamu; unatekeleza utendaji wako mwenyewe kwa wepesi wa moyo tu, bila kujali sana kuhusu matokeo sembuse kuhusu iwapo kunayo mikengeuko au makosa katika utendaji wako. Kwa njia hii, bila shaka utendaji wako unakosa usahihi na kukosa maadili. Kile kinachokosa hasa ni mantiki ya kawaida ya kibinadamu na dhamiri inayostahili, pamoja na pongezi ya Mungu na uthibitisho wa Roho Mtakatifu inakuwa rahisi sana kufuata njia yako tu. Aina hii ya kutenda ni kufuata sheria tu au kuchukua mzigo zaidi kimakusudi ili ujizuie na kujidhibiti. Ilhali unafikiri kuwa utendaji wako uko sahihi kabisa, bila kujua kwamba sehemu kubwa ya utendaji wako unahusu michakato au kanuni ambazo si za lazima. Kuna wengi ambao wanatenda hivi kwa miaka mingi hasabila mabadiliko katika tabia zao, bila ufahamu mpya, na bila kuingia kupya. Wanatenda tena makosa yale yale ya zamani bila kujua na kutekeleza asili zao za kinyama wapendavyo, hata hadi kiwango ambapo mara nyingi wanafanya matendo ya kinyama, yasiyo ya busara na kutenda kwa njia ambazo zinawaacha watu wakichanganyikiwa na kushangazwa kabisa. Je, watu kama hao wanaweza kusemwa kuwa wamepitia mabadiliko katika tabia?

Sasa, imani katika Mungu imeingia katika Enzi ya Neno la Mungu. Tukizungumza kwa kulinganisha, watu hawaombi kadiri walivyokuwa wakiomba awali; maneno ya Mungu yamewasilisha wazi vipengele vyote vya ukweli na njia za utendaji, kwa hivyo hakuna tena haja wa watu kujitahidi na kutafuta kwa kupapasa papasa. Katika maisha ya Enzi ya Ufalme, maneno ya Mungu yanawaongoza watu mbele, nayo ni maisha ambamo kila kitu kinaelezwa waziwazi kwao ili waone—kwa kuwa Mungu ameweka kila kitu wazi, na mwanadamu haachwi tena kutafuta njia katika maisha. Kuhusu ndoa, mambo ya kidunia, maisha, chakula, mavazi na malazi, mahusiano kati ya watu, jinsi mtu anavyoweza kuhudumu kwa njia ambayo inayakidhi mapenzi ya Mungu, jinsi mtu anavyopaswa kuunyima mwili, na kadhalika, Mungu hajawaelezea yepi kati ya mambo haya? Je, bado mnahitaji kwenda kuomba na kutafuta? Hakuna haja kweli! Kama bado unafanya mambo haya, unatenda tu kwa kupita kiasi. Huu ni ujinga na upumbavu, na hauhitajiki kabisa! Ni wale tu waliopungukiwa kabisa katika ubora wa tabia na wasioweza kuelewa maneno ya Mungu ndio wanaoomba maombi ya kipumbavu bila kukoma. Jambo la muhimu katika kuutekeleza ukweli ni kama una azimio au la. Baadhi ya watu wanasisitiza kufuata mambo ya kimwili wanayoyapendelea katika matendo yao hata kama wanapojua wazi kuwa hayapatani na ukweli. Hili basi linazuia kuendelea kwao wenyewe katika maisha, na hata baada ya kuomba na kutafuta bado wanataka kutenda kwa kuustahi mwili. Wanapofanya hivi, je, hawatendi dhambi kwa kujua? Kama wale wanaotamani anasa za mwili na kutamani pesa, na wale wamaomwomba Mungu baadaye, wakisema: “Mungu! Je, Utaniruhusu nitamani anasa za mwili na kutamani utajiri? Je, ni mapenzi Yako nipate fedha kwa njia hii?” Je, hii ni njia inayofaa ya kuomba? Watu wanaofanya hivi hujua vizuri kabisa kwamba Mungu hafurahii

mambo haya, na kwamba wanapaswa kuyaacha, lakini mambo wanayoyashikilia mioyoni mwao yameshaamuliwa, na wanapoomba na kutafuta wanajaribu kumlazimisha Mungu awaruhusu kutenda kwa namna hii. Mioyoni mwao, hata wanaweza kumtaka Mungu aseme jambo ili kuthibitisha hili—huu ndio unaoitwa uasi. Pia kuna wale ambao huwaleta ndugu wa kanisa kwa upande wao na kuanzisha falme zao huru wenyewe. Unajua vizuri sana kwamba matendo haya yanampinga Mungu, lakini pindi tu unapoazimia kutenda jambo kama hili bado unaenda kumtafuta na kumwomba Mungu kwa utulivu na bila hofu. Huna aibu hata kidogo! Kuhusu kuyaacha nyuma mambo ya kidunia, jambo hili lilizungumziwa zamani. Kuna baadhi ya watu wanaojua wazi kuwa Mungu anachukia mambo ya kidunia, lakini bado wanaomba, wakisema: “Ee Mungu! Ninaelewa kuwa Hutanikubalia niendeleo kutenda mambo ya kidunia, lakini ninafanya hili ili jina Lako lisiaibishwe; ninalifanya ili watu wa kidunia waweze kuona utukufu Wako ndani yangu.” Haya ni maombi ya aina gani? Mnaweza kujua? Ni aina ya maombi yanayokusudia kumlazimisha na kumshurutisha Mungu. Je, huoni aibu kuomba kwa namna hii? Watu wanaomba kwa namna hii humpinga Mungu kwa makusudi, na maombi ya aina hii ni suala la utata kabisa; ni maonyesho ya tabia ya kishetani kweli. Maneno ya Mungu yako dhahiri kabisa, hasa yale yanayonenwa kuhusiana na mapenzi Yake, tabia Yake, na jinsi Yeye huwatendea watu wa aina tofauti. Ikiwa huuelewi ukweli, basi unapaswa kuyasoma maneno ya Mungu zaidi—matokeo ya kufanya hivi ni bora zaidi kuliko kuomba na kutafuta bila kutafakari. Kuna nyakati nyingi ambapo kutafuta na kuomba kunapaswa kubadilishwa na kusoma maneno ya Mungu zaidi na kushiriki kuhusu ukweli. Katika maombi yako ya kawaida, unapaswa kutafakari na kujaribu kujijua zaidi kutoka ndani ya maneno ya Mungu. Hili ni lenye manufaa zaidi kwa ajili ya maendeleo yako katika maisha. Ikiwa, sasa, bado unatafuta kwa kuinua macho yako mbinguni, je, hiyo haionyeshi kuwa bado unamwamini Mungu asiye dhahiri? Awali, uliona matokeo kutokana na kutafuta na kuomba kwako na Roho Mtakatifu aligusa roho yako kwa kiasi fulani kwa sababu huo ulikuwa wakati wa Enzi ya Neema. Hukuweza kumwona Mungu, kwa hivyo hukuwa na chaguo ila kuitafuta njia yako kuelekea mbele na kutafuta kwa namna hiyo. Sasa Mungu amekuja kati ya wanadamu, Neno limeonekana katika mwili, na umemwona Mungu; kwa hiyo Roho Mtakatifu hafanyi kazi tena kama Alivyofanya mbeleni. Enzi imebadilika na pia namna ambavyo Roho Mtakatifu hufanya kazi imebadilika. Ingawa huenda watu hawaombi sana kama walivyofanya awali, kwa sababu Mungu yuko duniani, mwanadamu sasa anayo nafasi ya kumpenda Mungu. Wanadamu wameingia katika enzi ya kumpenda Mungu na wanaweza kwa kawaida kumkaribia Mungu vizuri zaidi ndani yao wenyewe: “Ee Mungu! Hakika Wewe ni mzuri sana, nami natamani kukupenda!” Maneno machache tu ya wazi na rahisi hudhihirisha upendo kwa Mungu ndani ya mioyo ya watu; ombi hili linasemwa tu kwa ajili ya kuimarisha upendo kati ya mwanadamu na Mungu. Wakati mwingine unaweza kujiona ukionyesha uasi kiasi, na kusema: “Ee Mungu! Mbona mimi ni mpotovu sana?” Unatamani sana

kujipiga mara kadhaa, na machozi yanakulengalenga. Katika nyakati kama hizi, unahisi kujuta na kuwa na dhiki moyoni mwako, lakini huna namna ya kuonyesha hisia hizi. Hii ndiyo kazi ya sasa ya Roho Mtakatifu, lakini ni wale tu wanaofuatilia maisha ndio wanaoweza kuifikia. Unahisi kwamba Mungu anakupenda sana nawe unao hisia maalum. Ingawa huna maneno ya kuomba kwa uwazi, daima unahisi kwamba upendo wa Mungu ni wa kina kama bahari. Hakuna maneno sahihi ya kuonyesha hali hii, na hali hii ndiyo hutokea mara nyingi rohoni. Maombi na ushirika wa aina hii, yanayolenga kumvuta mtu karibu na Mungu moyoni mwake, ni ya kawaida.

Ingawa wakati ambao watu walibabaika na kutafuta sasa umepita, hilo halimaanishi kwamba hawastahili kuomba kutafuta tena, wala si kwamba watu hawahitaji kuyasubiri mapenzi ya Mungu yajifichue kabla ya kuendelea na kazi; huku ni kuelewa mambo tu kwa mwanadamu. Mungu amekuja miongoni mwa wanadamu ili Aishi nao, awe mwanga wao, maisha yao na njia yao: Huu ni ukweli. Bila shaka, katika kuja kwa Mungu duniani, kwa kweli Yeye huwaletoa wanadamu njia na maisha ya vitendo ambayo yanafaa kimo chao kwa ajili yao kufurahia—Hajaja kuharibu njia zote za matendo ya mwanadamu. Mwanadamu haishi tena kwa kupapasapapasa na kutafuta kwa sababu mambo haya yamebadilishwa na Mungu kuja duniani ili kufanya kazi na kunena neno Lake. Amekuja kumweka mwanadamu huru kutoka kwa maisha ya giza na mashaka ambayo amekuwa akiishi na kumwezesha awe na maisha yaliyojawa mwanga. Kazi ya sasa ni ya kuonyesha mambo kwa uwazi, kusema kwa uwazi, kufahamisha moja kwa moja, na kufafanua mambo haya waziwazi, ili watu waweze kuyaweka mambo haya katika matendo, jinsi Yehova Mungu alivyowaongoza watu wa Israeli, Akiwaambia jinsi ya kutoa sadaka na jinsi ya kulijenga hekalu. Kwa hiyo, hakuna haja tena ya ninyi kuishi maisha ya kutafuta kwa dhati kama mlivyofanya baada ya Bwana Yesu kuondoka. Je, mnapaswa kuihisi njia yenu kupitia kazi ya kueneza injili katika siku za baadaye? Je, mnapaswa kupapasapapasa mkijaribu kutafuta njia mwafaka ya kuishi? Je, mnapaswa kupapasa papasa ili mtambue jinsi mnavyofaa kutekeleza wajibu wenu wenyewe? Je, ni lazima ninyi msujudu ardhini na kutafuta, ili mjue jinsi mnavyopaswa kushuhudia? Je, ni lazima ninyi mfunge na kuomba ili mjue jinsi mnavyopaswa kuvaa au kuishi? Je, ni lazima ninyi muombe kwa Mungu aliye mbinguni bila kukoma ili mjue jinsi mnavyopaswa kukubali kushindwa na Mungu? Je, ni lazima muombe bila kukoma, usiku na mchana, ili mjue jinsi mnavyopaswa kumtii Mungu? Kuna wengi miongoni mwenu wanaosema kwamba hamwezi kutenda kwa sababu hamwelewi. Watu hawaizingatii kazi ya Mungu siku hizi hata kidogo! Nilisema maneno mengi muda mrefu uliopita, lakini hamkuwahi kuzingatia kuyasoma hata kidogo, hivyo si ajabu kwamba hamjui jinsi ya kutenda. Bila shaka, katika enzi ya leo Roho Mtakatifu bado Huwagusa watu ili kuwasababisha wahisi starehe, Naye anaishi pamoja na mwanadamu. Hiki ndicho chanzo cha hisia hizo^[a] maalum zenye kuanisi ambazo mara nyingi hutokea katika maisha yako. Kila baada ya muda fulani, siku huja

ambapo unahisi kwamba Mungu ni wa kupendeza sana nawe huwezi kujizuia kumwomba: “Ee Mungu! Upendo Wako ni mzuri sana na sura Yako ni nzuri sana. Natamani kukupenda kwa undani zaidi. Natamani kujitoa kabisa ili kuyatumia maisha yangu yote. Nitatoa kila kitu Kwako, mradi ni kwa ajili Yako, mradi kwa kufanya hivi ninaweza kukupenda....” Hii ni hisia ya furaha uliyopewa na Roho Mtakatifu. Si nuru, wala si mwangaza; ni uzoefu wa kuguswa. Uzoefu unaofanana na huu utatokea mara kwa mara: Wakati mwingine unapoelekea kazini, utaomba na kumkaribia Mungu, nawe utasisimuliwa hadi kiwango ambapo machozi yataulowesha uso wako na hutaweza kujidhibiti, nawe utakuwa na hamu ya kupata mahali pa kufaa ambapo unaweza kuonyesha hamasa zote zilizo moyoni mwako.... Kutakuwa na nyakati utakapokuwa hadharani na utahisi kwamba unaufurahia upendo mwingi mno wa Mungu, kwamba bahati yako si ya kawaida, na hata zaidi kwamba unaishi maisha yako na kusudi zaidi kuliko mtu mwingine yeyote. Utajua kwa undani zaidi kwamba Mungu amekuinua, na kwamba huu ni upendo mkuu wa Mungu kwako. Katika maficho ya ndani kabisa ya moyo wako utahisi kuwa kuna upendo fulani ndani ya Mungu usioweza kuonyeshwa na usioweza kueleweka kwa mwanadamu, kana kwamba unaujua lakini huna namna ya kuueleza, ukikufanya ufikirie kwa makini siku zote lakini ukikuacha usiweze kuuonyesha kabisa. Wakati kama huu, hata utasahau ulipo, nawe utaita: “Ee Mungu! Wewe huwezi kueleweka nawe Unapendwa sana!” Hili litawaacha watu kwa mshangao, lakini hayo yote hutendeka mara kwa mara. Nyinyi mmepitia mambo kama haya mara nyingi sana. Haya ndiyo maisha ambayo Roho Mtakatifu amekupa leo na maisha ambayo unapaswa kuishi sasa. Jambo hili halinui kukufanya uache kuishi maisha, bali kubadilisha jinsi unavyoishi maisha yako. Ni hisia ambayo haiwezi kuelezeka au kuonyeshwa. Pia ndiyo hisia ya kweli ya mwanadamu na hata zaidi ndiyo kazi ya Roho Mtakatifu. Unaweza kuelewa katika moyo wako, lakini huna namna ya kuionyesha wazi kwa mtu yeyote hata kidogo. Hii si kwa sababu wewe si mwepesi wa kusema au kwamba wewe ni kigugumizi, lakini kwa sababu ni aina ya hisia ambayo haiwezi kuelezwa katika maneno. Unaruhusiwa kufurahia mambo haya leo, na haya ndiyo maisha unayopaswa kuishi. Bila shaka, vipengele vingine vya maisha yako haviko tupu; ni kwamba tu uzoefu huu wa kulisimuliwa unakuwa aina ya furaha katika maisha yako ambao unakufanya utake kufurahia uzoefu kama huo kutoka kwa Roho Mtakatifu siku zote. Lakini unapaswa kujua kwamba kuguswa kwa namna hii hakufanyiki ili uweze kuuzidi mwili na kwenda katika mbingu ya tatu au kusafiri kote duniani. Badala yake, ni ili uweze kuhisi na kuonja upendo wa Mungu ambao unafurahia leo, upate uzoefu wa umuhimu wa kazi ya Mungu leo na ufahamiane tena na utunzaji na ulinzi wa Mungu. Mambo haya yote ni ili upate kuwa na maarifa zaidi ya kazi ambayo Mungu hufanya leo—hili ndilo lengo katika kufanya kazi hii.

Kutafuta na kupapasa papasa ilikuwa ndiyo namna ya maisha kabla ya Mungu kupata mwili. Wakati huo watu hawakuweza kumwona Mungu na hivyo hawakuwa na chaguo ila

kutafuta na kupapasa papasa. Leo umemwona Mungu naye Anakwambia moja kwa moja jinsi unavyopaswa kutenda; hii ndiyo sababu huhitaji tena kupapasa papasa au kutafuta. Njia ambayo Anamwongoza mwanadamu ni njia ya ukweli, na mambo Anayomwelezea mwanadamu na ambayo mwanadamu anapokea ni maisha na ukweli. Unayo njia, uzima na ukweli, hivyo kuna haja gani ya kutafuta kila mahali? Roho Mtakatifu hatatenda hatua mbili za kazi kwa pamoja. Ikiwa, wakati Nimemaliza kunena neno Langu, watu hawali na kunywa neno la Mungu kwa uangalifu na kuufuatilia ukweli ifaavyo, bado wakitenda jinsi walivyotenda katika Enzi ya Neema, wakipapasapapasa kana kwamba wao ni vipofu, wakiomba na kutafuta siku zote, hiyo haitamaanisha kwamba hatua hii ya kazi Yangu—kazi ya maneno—inafanywa bure? Ingawa Naweza kuwa Nimemaliza kunena neno Langu, watu bado hawaelewi kabisa, na hii ni kwa sababu wamekosa ubora wa tabia. Tatizo hili linaweza kutatuliwa kwa kuishi maisha ya kanisa na kupitia kushiriki sisi kwa sisi. Awali, katika Enzi ya Neema, ingawa Mungu alikuwa mwili, hakufanya kazi ya maneno, ambayo ndiyo sababu Roho Mtakatifu alifanya kazi kwa njia hiyo wakati huo ili kuidumisha kazi. Wakati huo ilikuwa hasa Roho Mtakatifu aliyeifanya kazi, lakini sasa ni Mungu mwenye mwili Mwenyewe ambaye Anaifanya, baada ya kuchukua nafasi ya kazi ya Roho Mtakatifu. Awali, mradi watu waliomba mara kwa mara, walipata amani na furaha; kulikuwa na lawama pamoja na nidhamu. Hii yote ilikuwa kazi ya Roho Mtakatifu. Sasa hali hizi ni chache na nadra. Roho Mtakatifu anaweza tu kufanya aina moja ya kazi katika enzi yoyote ile. Kama Angefanya aina mbili za kazi wakati huo huo, mwili ukifanya aina moja na Roho Mtakatifu akifanya aina nyingine ndani ya watu, na kama kile mwili ulisema hakikuwa na thamani na kile Roho alifanya ndicho kilikuwa na thamani tu, basi Kristo asingekuwa na ukweli wowote, njia au uzima wowote hata kidogo. Huku kungekuwa kujipinga na kungekuwa makosa katika chanzo chake kabisa. Roho Mtakatifu anaweza kutenda kwa njia hii? Mungu ni mwenyezi na mwenye hekima yote, mtakatifu na mwenye haki, na Hatendi makosa yoyote kamwe.

Kulikuwa na mikengeuko na makosa mengi mno katika uzoefu wa zamani wa watu. Kulikuwa na mambo fulani ambayo watu wa ubinadamu wa kawaida walikuwa wamenuiwa kuwa nayo au kufanya, au kulikuwa na makosa ambayo yalikuwa magumu kuepuka katika maisha ya binadamu, na wakati mambo hayo yalishughulikiwa vibaya, watu walimlaumu Mungu. Kulikuwa na dada ambaye alikuwa na wageni nyumbani kwake. Maandazi yake ya kuchemshwa hayakuchemshwa vyema, hivyo akafikiri: “Labda hii ni nidhamu ya Mungu. Mungu anaughulika moyo wangu usiofaa tena; kiburi changu kweli ni kibubwa mno.” Kwa kweli, tukizingatia jinsi mwanadamu hufikiria kwa kawaida, wageni wanapokuja, unasisimka na kukimbia huku na kule, bila kuwa na utaratibu katika kila kitu unachofanya, na kwa hiyo bila shaka wali utaungua au vyakula vitaishia kuwa na chumvi nyingi sana. Hii hutokea kwa sababu ya kuisimka sana, lakini watu huishia kudhania kuwa ni “nidhamu ya Mungu.” Kwa kweli, haya

yote ni makosa tu yanayotendwa katika maisha ya binadamu. Je, hungekumbana pia na aina hii ya jambo mara kwa mara iwapo hungemwamini Mungu? Shida ambazo hutokea mara nyingi hutokana na makosa yaliyotendwa na watu—haiwezekani kabisa kwamba makosa kama haya yametendwa na Roho Mtakatifu. Makosa kama haya hayamhusu Mungu. Kwa mfano unapojiuma ulimi unapokula—hiyo inaweza kuwa ni nidhamu ya Mungu? Nidhamu ya Mungu ina kanuni na kwa kawaida huonekana wakati unatenda kosa kwa kujua. Ni wakati tu unatenda mambo yanayohusu jina la Mungu ama yanayohusu ushuhuda au kazi Yake ndipo Atakufundisha nidhamu. Watu wana ufahamu wa ndani wa mambo wanayoyafanya kwa sababu wanaelewa ukweli vya kutosha sasa. Kwa mfano: Je, unaweza kutohisi chochote ukibadhiri fedha za kanisa au kuzitumia bila kujali? Utahisi jambo unapofanya hivyo. Haiwezekani tu kuhisi jambo fulani kitendo kitakapokuwa kishafanywa. Unaelewa moyoni mwako kuhusu mambo unayoyatenda yanayoenda kinyume na dhamiri yako. Kwa kuwa watu wanayo mambo yao wenyewe wanayoyapenda au kuyapendelea, wao hujifurahisha tu ingawa wanajua wazi jinsi ya kuuweka ukweli katika vitendo. Hivyo, baada ya wao kutenda jambo, hawahisi shutuma yoyote au kupitia nidhamu yoyote dhahiri. Hii ni kwa sababu wametenda kosa kwa makusudi, kwa hiyo Mungu hawafundishi nidhamu; mara tu wakati wa hukumu ya haki ufikapo, adhabu ya Mungu italetwa juu ya kila mmoja kulingana na matendo yake. Kwa sasa kunao baadhi ya watu kanisani ambao hubadhiri fedha, baadhi wasioweka mipaka dhahiri kati ya wanaume na wanawake, na baadhi wanaohukumu, kupinga na kujaribu kuiharibu kazi ya Mungu kwa siri. Kwa nini bado kila kitu kiko sawa nao? Wanapotenda mambo kama hayo, wanao ufahamu na wanahisi aibu mioyoni mwao na kwa sababu ya hii, wakati mwingine wanaadibiwa na kutakaswa, lakini wao hawana aibu hata kidogo! Jinsi tu watu wanaposhiriki katika uzinzi—wanajua wanachokifanya wakati huo, lakini tamaa yao ni kubwa mno na hawawezi kujidhibiti. Hata Roho Mtakatifu akiwafundisha nidhamu, itakuwa bure, kwa hiyo Roho Mtakatifu hatafundisha nidhamu. Roho Mtakatifu asipowafundisha nidhamu wakati huo, wasipohisi shutuma yoyote na hakuna chochote kinachotendekeza miili yako, kutakuwa na shutuma gani baadaye? Kitendo kimefanyika—kutakuwa na nidhamu gani? Inathibitisha tu kwamba hawana aibu kabisa nao wamepungukiwa na ubinadamu, na kwamba wanastahili laana na adhabu! Roho Mtakatifu hafanyi kazi bila sababu. Ikiwa unaujua ukweli vizuri sana lakini huutii katika vitendo, ikiwa unaweza kutenda uovu wowote, basi unachoweza kusubiri tu ni kuwasili kwa siku ile ambapo utaadhibiwa pamoja na yule mwovu. Huu ndio mwisho bora kwako! Sasa Nimehubiri nikirudia kuhusu dhamiri, ambacho ni kigezo cha chini kabisa. Watu wakikosa dhamiri, basi wamepoteza nidhamu ya Roho Mtakatifu; wanaweza kufanya chochote wanachotaka na Mungu hawazingatii. Wale ambao kwa kweli wana dhamiri na mantiki wataifahamu wanapotenda jambo baya. Watahisi wasiwasi mara tu wanapohisi shutuma kidogo katika dhamiri yao; watapitia pigano la ndani na mwishowe kuutelekeza mwili. Hawatafika kiwango ambapo wanatenda

jambo linalompinga Mungu pakubwa. Haijalishi ikiwa Roho Mtakatifu anafundisha nidhamu na kuwaadibu, watu wote watakuwa na hisia fulani wanapotenda jambo baya. Kwa hiyo, watu sasa wanaelewa aina zote za ukweli na kama hawautendi basi hilo ni suala la kibinadamu. Siwajibu watu kama hawa hata kidogo, wala siwaonei tumaini lolote. Unaweza kufanya utakavyo!

Watu wengine wanapokuja pamoja, wanaliweka neno la Mungu upande mmoja na daima wanazungumza kuhusu jinsi mtu huyu au mtu yule alivyo. Bila shaka ni vizuri kuwa na utambuzi kidogo, ili bila kujali unapokwenda hutadanganywa kwa urahisi, wala hautalaghaiwa au kupumbazwa kwa urahisi—hiki pia ni kipengele ambacho watu wanapaswa kumiliki. Lakini usilenge tu suala hili. Hii inahusiana na upande mbaya wa mambo, na huwezi kuwakazia watu wengine macho daima. Unao ufahamu kidogo sana sasa kuhusu jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi, imani yako katika Mungu ni ya juujuu sana, nawe unayo mambo machache mno yaliyo mazuri. Yule unayemwamini ni Mungu, na Yule unayehitaji kumwelewa ni Mungu, si Shetani. Ikiwa unatambua tu jinsi Shetani anavyofanya kazi na njia zote ambazo kwazo roho mbaya zinafanya kazi, lakini huna ufahamu wa Mungu hata kidogo, hiyo itakuwa na maana gani? Je, si ni Mungu unayemwamini leo? Kwa nini ufahamu wako hauhusishi mambo haya mazuri? Hutilii maanani kipengele kizuri cha kuingia hata kidogo, wala hukifahamu, hivyo ni nini hasa unachotaka kupata katika imani yako? Je, hujui jinsi unavyopaswa kufuatilia? Unajua mengi kuhusu vipengele vilivyo hasi, lakini unaambulia patupu kuhusu kipengele kizuri cha kuingia, kwa hiyo kimo chako kitawezaje kuwahi kukua? Mtu kama wewe anayezungumza tu kuhusu vita na Shetani atakuwa na matarajio yapi ya baadaye ya maendeleo? Kuingia kwako hakutakuwa kumepitwa na wakati sana? Utaweza kupata nini kutokana na kazi ya sasa kwa kufanya hili? Kilicho muhimu sasa ni wewe uelewe nini Mungu anataka kufanya sasa, jinsi binadamu wanavyopaswa kushirikiana, jinsi wanavyopaswa kumpenda Mungu, jinsi wanavyopaswa kuelewa kazi ya Roho Mtakatifu, jinsi wanavyopaswa kuingia katika maneno yote ambayo Mungu anasema leo, jinsi wanavyopaswa kuyala na kuyanywa, kuyapitia, na kuyaelewa, jinsi yanavyopaswa kuyakidhi mapenzi ya Mungu, washindwe kabisa na Mungu na kumtii Mungu.... Haya ndiyo mambo unayopaswa kuyalenga na yanayopaswa kuingiwa sasa. Je, unaelewa? Kuna faida gani kulenga tu utambuzi wa watu wengine? Unaweza kumtambua Shetani hapa, kuzitambua roho mbaya huko—unaweza kuwa na ufahamu kamili wa roho mbaya, lakini kama huwezi kusema chochote kuhusu kazi ya Mungu, je, utambuzi kama huo unaweza kuchukua nafasi ya kumfahamu Mungu? Hapo awali Nimeshiriki kuhusu maonyesho ya kazi ya roho mbaya, lakini hili halijakuwa sehemu kubwa ya ushirika huo. Bila shaka watu wanapaswa kuwa na ufahamu kiasi na hiki ni kipengele ambacho wale wanaomtumikia Mungu wanapaswa kumiliki ili kuepuka kufanya mambo ya kipuuzi na kuikatiza kazi ya Mungu. Hata hivyo, jambo muhimu zaidi linabaki kuwa na maarifa ya kazi ya Mungu na kuelewa mapenzi ya Mungu. Ni

ufahamu gani kuhusu hatua hii ya kazi ya Mungu iko ndani yako? Je, unaweza kuzungumza kuhusu kile ambacho Mungu hufanya, mapenzi ya Mungu ni yepi, mapungufu yako ni yapi na mambo unayopaswa kujiandaa nayo? Je, unaweza kusema kuingia kwako kupya zaidi ni kupi? Unapaswa kuweza kuvuna matunda na kutimiza ufahamu katika kuingia huko kupya. Usijifanye kuwa na kiwewe; lazima ufanye juhudi zaidi katika kuingia huko kupya ili uimarishe uzoefu na ufahamu wako mwenyewe, na hata zaidi lazima upate ufahamu wa kuingia kupya zaidi kwa sasa na njia sahihi zaidi ya kupata uzoefu. Aidha, kupitia kazi na kuingia kupya, lazima uwe na utambuzi kuhusu mazoea yako ya zamani yaliyopitwa na wakati na yaliyopotoka, na utafute jinsi ya kuyatupilia mbali ili uingie katika uzoefu mpya. Haya ni mambo ambayo sasa unahitaji kuyaelewa na kuingia ndani yake kwa haraka. Lazima uelewe tofauti na uhusiano kati ya kuingia kwa zamani na kuingia kupya. Kama huna ufahamu wa mambo haya, basi hutakuwa na njia yoyote ya kuendelea, kwa kuwa hutaweza kuendelea sambamba na kazi ya Roho Mtakatifu. Lazima uweze kula na kunywa kwa kawaida maneno ya Mungu na kufanya ushirika wa kawaida, na kuyatumia kubadilisha njia zako za zamani za kutenda na fikira zako za desturi za jadi, ili uweze kuingia katika utendaji upya, na kuingia katika kazi mpya ya Mungu. Haya ni mambo unayopaswa kutimiza. Sikusihi tu sasa uelewe hasa kama una sifa zinazostahili; hili silo lengo. Badala yake Ninakusihi kuchukulia kwa makini kutenda kwako ukweli na kuelewa kwako kuhusu kuingia katika maisha. Uwezo wako wa kujijua si mfano wa kimo chako cha kweli. Ikiwa unaweza kupitia kazi ya Mungu, upitie na kuelewa ukweli ndani ya maneno ya Mungu, na uweze kutambua fikira na makosa yako ya awali, basi hiki ni kimo chako cha kweli nacho ni kitu ambacho kila mmoja wenu anapaswa kutimiza.

Kuna hali nyingi ambamo ninyi hamjui hasa jinsi ya kutenda, sembuse kujua jinsi Roho Mtakatifu anavyofanya kazi. Wakati mwingine unatenda jambo ambalo ni dhahiri kwamba halimtii Roho Mtakatifu. Kupitia wewe kula na kunywa maneno ya Mungu, tayari unao ufahamu wa kanuni iliyo karibu katika suala hilo, kwa hiyo unayo hisia ya ndani ya lawama na kufadhaika; bila shaka hii ni hisia ambayo mtu atahisi tu kwa kigezo cha kujua ukweli fulani. Watu wasiposhirikiana au kutenda kulingana na neno la Mungu la leo, basi wanaipinga kazi ya Roho Mtakatifu na hakika watahisi kufadhaika ndani yao. Huenda unaelewa kanuni ya kipengele fulani lakini hutendi ipasavyo, kwa hiyo utapata hisia ya lawama ndani yako. Ikiwa huelewi kanuni hiyo na hujui kipengele hiki cha ukweli hata kidogo, basi haimaanishi kuwa lazima utahisi lawama kuhusu suala hili. Lawama ya Roho Mtakatifu huwa katika maudhui yanayofaa daima. Unafikiri kwamba kwa kuwa hujaomba na hujashirikiana na kazi ya Roho Mtakatifu kwamba umeichelewesha kazi. Kwa hakika, haiwezi kuchelewesha. Roho Mtakatifu atamgusa mtu mwingine; kazi ya Roho Mtakatifu haizuiliwi na yeyote. Unahisi kwamba umemtahayarisha Mungu, na hii ndiyo hisia unayopaswa kuwa nayo katika dhamiri yako. Kama unaweza kuupata

ukweli au la ni shauri yako mwenyewe na haihusiani na Mungu. Wakati mwingine ni dhamiri yako mwenyewe inayohisi kushutumiwa, lakini hii si nuru au mwangaza wa Roho Mtakatifu, wala si lawama ya Roho Mtakatifu. Badala yake ni hisia iliyo ndani ya dhamiri ya mwanadamu. Ukitenda kwa utukutu katika mambo yanayohusu jina la Mungu, ushuhuda wa Mungu au kazi ya Mungu, basi Mungu hatakuachilia. Lakini kuna mpaka—Mungu hatajishughulisha nawe katika mambo madogo ya kawaida. Atakupuuza. Ukikiuka kanuni, na uivuruge kazi ya Mungu, utakabiliwa na ghadhabu Yake na hatakuachilia kabisa. Baadhi ya makosa unayoyatenda hayawezi kuepukika katika maisha ya binadamu. Kwa mfano, huchemshi maandazi kwa njia ifaayo na kusema kuwa ni Mungu anakufundisha nidhamu—hili ni jambo lisilo na mantiki kabisa kusema. Kabla ya kuja kumwamini Mungu, jambo la aina hii halikutokea mara nyingi? Unahisi kwamba inaonekana kuwa nidhamu ya Roho Mtakatifu, lakini kwa kweli hivi sivyo ilivyo (bila kuzingatia baadhi ya hali za kipekee), kwa sababu kazi hii haitoki kwa Roho Mtakatifu kabisa, lakini badala yake inatokana na hisia za binadamu. Hata hivyo, ni kawaida kwa watu walio na imani kufikiria kwa namna hii. Hungeweza kufikiria hivi wakati ambapo hukumwamini Mungu. Mara ulipokuja kumwamini Mungu, ulianza kutumia muda mwingi ukitafakari mambo haya na kwa hiyo kwa kawaida ulifikiri kwa namna hii. Hili linatokana na mawazo ya kawaida ya watu na linahusiana na akili zao. Lakini hebu Nikwambie, kufikiri kwa aina hii hakuko katika eneo la kazi ya Roho Mtakatifu. Huu ni mfano wa Roho Mtakatifu kuwapa watu mjibizo wa kawaida kupitia mawazo yao; lakini lazima uelewe kwamba mjibizo huu si kazi ya Roho Mtakatifu. Kuwa na aina hii ya “maarifa” hakuthibitishi kwamba unayo kazi ya Roho Mtakatifu. Maarifa yako hayatokani na nuru ya Roho Mtakatifu, sembuse kazi ya Roho Mtakatifu. Ni matokeo ya wazo la kawaida kibinadamu tu na hayahusiani kamwe na nuru au mwanga wa Roho Mtakatifu—bila shaka haya ni mambo mawili tofauti kabisa. Wazo la kawaida kama hili la kibinadamu halitoki kwa Roho Mtakatifu kikamilifu. Roho Mtakatifu anapofanya kazi ili kuwapa watu nuru, kwa ujumla Yeye huwapa ufahamu wa kazi ya Mungu, na ufahamu wa kuingia kwao kwa kweli na hali yao ya kweli. Yeye pia huwasababisha waelewe nia za dharura za Mungu na madai Yake kwa mwanadamu leo, ili wawe na azimio la kudhabihu kila kitu ili wamridhishe Mungu, wampende Mungu hata wakikumbana na mateso na dhiki, na kuwa shahidi kwa Mungu hata ikimaanisha kumwaga damu yao au kutoa maisha yao, na kufanya hivyo bila majuto. Ukiwa na azimio la aina hii, inamaanisha unayo misisimko na kazi ya Roho Mtakatifu—lakini jua kwamba huna misismko ya aina hii kila wakati. Wakati mwingine katika mikutano unapoomba na kula na kunywa maneno ya Mungu, unaweza kuhisi kuguswa na kupata msukumo mno. Linaonekana jambo la kuburudisha kabisa wakati watu wengine wanashiriki baadhi ya uzoefu na ufahamu wao wa maneno ya Mungu, na moyo wako uko wazi na mchangamfu kabisa. Hii yote ni kazi ya Roho Mtakatifu. Kama wewe ni kiongozi na Roho Mtakatifu anakupa nuru na mwangaza usio wa kawaida unapoenda kanisani kufanya kazi,

Anakupa umaizi wa shida ambazo zipo katika kanisa, Anakuwezesha kujua jinsi ya kushiriki kuhusu ukweli ili kuzitatua, Anakufanya uwe mwenye bidii ya ajabu sana, mwenye kuwajibika na uliye makini katika kazi yako, hii yote ni kazi ya Roho Mtakatifu.

Tanbihi:

a. Maandiko ya asili yanasoma “Hizi ni baadhi”

Utendaji (2)

Katika nyakati zilizopita, watu walijifunza wenyewe kuwa na Mungu na kuishi ndani ya roho kila wakati. Ukilinganishwa na utendaji wa leo, hayo ni mafundisho rahisi ya kiroho, ni mbinu ya juujuu zaidi na rahisi zaidi ya utendaji kabla ya watu kuingia kwenye njia sahihi ya maisha, na yanaunda hatua ya kwanza kabisa ya utendaji katika imani ya watu. Ikiwa watu watategemea utendaji wa aina hii maishani mwao kila mara, watakuwa na hisia nyingi na huenda wakafanya makosa na hawatakuwa na uwezo wa kuingia katika uzoefu wa kweli wa maisha; wataweza tu kuzifundisha roho zao, kumkaribia Mungu kwa kawaida katika mioyo yao, na kila mara watapata furaha nyingi mno katika kuwa na Mungu pamoja nao. Watajiwekea mipaka katika mawanda madogo ya upamoja wao na Mungu, na hawataweza kufikia kitu chochote cha kina zaidi. Watu ambao huishi katika mipaka hii hawana uwezo wa kupiga hatua yoyote kubwa. Wakati wowote, wanaweza kupaza sauti, “Ee! Bwana Yesu. Amina!” Wako hivi takribani kila siku—ni utendaji wa nyakati zilizopita, utendaji wa kuishi ndani ya roho kila wakati. Huo sio utovu wa adabu? Leo, ufikapo wakati wa kutafakari maneno ya Mungu, zingatia tu kutafakari maneno ya Mungu; ufikapo wakati wa kuuweka ukweli katika vitendo, zingatia tu kuuweka ukweli katika vitendo; na ufikapo wakati wa kutekeleza wajibu wako, tekeleza tu wajibu wako. Utendaji wa aina hii kwa kweli utakuweka huru; unakufungua wewe. Sio kama jinsi wazee wa dini huomba na kusema sala ya mlo. Bila shaka, hapo awali, watu wa imani walitenda hivi, lakini sasa kutenda kwa namna hii ni kuwa nyuma kimaendeleo. Kazi ya Mungu sasa iko katika kiwango cha juu zaidi; kinachozungumziwa leo, “kumleta Mungu katika maisha halisi,” ndicho kipengele muhimu zaidi cha utendaji. Huu ndio ubinadamu wa kawaida ambao watu wanatarajiwa kumiliki katika maisha yao halisi, na kile ambacho watu wanapaswa kuwa nacho katika ubinadamu wao wa kawaida ni maneno yote ambayo Mungu ananena leo. Kuyaleta maneno haya ya Mungu katika maisha ya kweli ndiyo maana halisi ya “kumleta Mungu katika maisha halisi.” Leo, watu wanapaswa hasa kujiandaa na yafuatayo: Kwa upande mmoja, lazima waboreshe ubora wao wa tabia, wapate mafunzo na waboreshe ustadi wao wa usomaji na uelewaji; na katika mwingine, lazima waishi maisha ya mtu wa kawaida. Umerudi tu mbele ya Mungu kutoka ulimwenguni; lazima kwanza ufunze moyo wako kutulia mbele ya Mungu. Huu ndio mwanzo kabisa wa utendaji, na pia ndiyo hatua ya kwanza ya kutimiza mabadiliko katika

tabia yako ya maisha. Watu wengine kwa ulinganisho ni wepesi kubadilika katika utendaji wao; wao hutafakari ukweli huku wakifanya kazi, wakijaribu kuelewa ukweli na kanuni za utendaji wanazopaswa kufahamu kwa uhalisi. Kipengele kimoja ni kwamba lazima uwe na maisha ya kawaida ya binadamu, na kingine ni kwamba lazima kuwe na kuingia katika ukweli. Vitu hivi vyote vinajumuisha utendaji bora zaidi wa maisha halisi.

Kumleta Mungu katika maisha halisi ya watu kimsingi kunahitaji kwamba wamwabudu Mungu, watafute kumjua Mungu, na kutekeleza wajibu wa kiumbe wa Mungu ndani ya ubinadamu wa kawaida. Sio kwamba ni lazima wamwombe Mungu kila wakati wanapofanya kitu, kwamba si sawa na kwamba wanapaswa kuhisi ni wadeni Wake wasipoomba. Utendaji wa leo si namna hiyo; ni rahisi sana! Hauwahitaji watu wafuate kanuni. Badala yake, kila mtu anapaswa kutenda kulingana na kimo chake mwenyewe: Ikiwa wanafamilia wako hawamwamini Mungu, wachukulie kama watu wasioamini, na ikiwa wanaamini, wachukulie kama waumini. Usitende kwa upendo na uvumilivu, badala yake tenda kwa hekima. Watu wengine huenda kununua mboga, na huku wakitembea wao hunong'ona: "Ee Mungu! Ni mboga gani ambazo Ugependa ninunue leo? Naomba usaidizi Wako. Mungu anataka tulitukuze jina Lake katika mambo yote na kwamba sote tuwe na ushuhuda, kwa hiyo hata muuzaji akinipa kitu kilichooza, bado nitampa Mungu shukrani—nitavumilia. Sisi tunaomwamini Mungu hatuwezi kuchagua kati ya mboga." Wanafikiria kwamba kufanya hivi ni ushuhuda, na matokeo ni kwamba wanatumia pesa kununua kibunda cha mboga zilizooza, lakini bado wanaomba na kusema: "Ee Mungu! Bado nitakula mboga hizi zilizooza alimradi Unikubali nifanye jambo hilo." Je, utendaji kama huo sio wa kipumbavu? Je, huko si kufuata mafundisho ya dini? Hapo awali, watu walijifunza kuishi ndani ya roho kila wakati—hili linahusiana na kazi iliyofanywa awali katika Enzi ya Neema. Uchaji Mungu, unyenyekevu, upendo, uvumilivu, kutoa shukrani kwa ajili ya mambo yote—haya ndiyo yale yaliyohitajika kutoka kwa kila muumini katika Enzi ya Neema. Wakati huo, watu walimwomba Mungu katika mambo yote; wangeomba waliponunua nguo, na walipofahamishwa juu ya mkutano, wangeomba pia na kusema: "Ee Mungu! Je, Utanikubalia niende au la? Ikiwa Utanikubalia niende, basi nitayarishie njia iliyonyooka. Ikiwa hutanikubalia niende, nifanye nijikwae na nianguke." Wangemsihi Mungu huku wakiomba, na baada ya kuomba wangehisi wasio na utulivu na wangekosa kwenda. Akina dada wengine, wakihofia kwamba baada ya kurudi nyumbani kutoka mikutanoni wanaweza kupigwa na waume wao wasioamini, walihisi wasio na utulivu walipoomba na kwa hivyo hawangeenda kwenye mikutano. Waliamini haya kuwa mapenzi ya Mungu, ilhali ukweli ni kwamba, iwapo wangeenda, hakuna chochote ambacho kingefanyika. Matokeo ni kwamba hawakuhudhuria mkutano. Haya yote yalikuwa matokeo ya ujinga wa watu. Watu wanaotenda kwa njia hii huishi kulingana na hisia zao wenyewe. Njia hii ya utendaji ni yenye makosa na ya kipumbavu sana na

imejaa hali ya kutokuwa yakini. Kuna hisia na mawazo yao binafsi mengi sana. Ukiambiwa kuhusu mkutano, basi nenda; hakuna haja zaidi ya kumwomba Mungu. Je, hili si jambo rahisi? Ikiwa unahitaji kununua mavazi fulani leo, basi nenda ukafanye hivyo. Usimwombe Mungu na kusema: “Ee Mungu! Utanikubalia niende au la? Na, je, ndugu au dada mmoja akija hapa nikiwa nimeondoka?” Unahofia huenda ndugu au dada fulani atakuja kwa hivyo huendi, ilhali matokeo ni kwamba jioni inafika na hakuna aliyekuja. Hata katika Enzi ya Neema, njia hii ya utendaji ilikuwa potovu na yenye makosa. Hivyo, watu wakitenda kama katika nyakati zilizopita, hakutakuwa na mabadiliko katika maisha yao. Kwa ujinga watakubali tu chochote kitakachotokea, hawatazingatia utambuzi na hawatafanya lolote ila kutii na kuvumilia pasipo kufikiria. Wakati huo, watu walilenga kumtukuza Mungu—lakini Mungu hakupata utukufu wowote kutoka kwao, kwani hawakuwa wameishi kwa kudhihirisha lolote la vitendo. Walijizuilia tu na kujiwekea mipaka kulingana na mawazo yao wenyewe, na hata miaka mingi ya utendaji haikuleta mabadiliko katika maisha yao. Walijua tu kuvumilia, kuwa wanyenyekevu, kupenda, na kusamehe, lakini hawakuwa na kiwango hata kidogo cha nuru kutoka kwa Roho Mtakatifu. Watu wangemjuaje Mungu kwa njia hiyo? Na wangewezaje kumtukuza Mungu?

Watu wanaweza tu kuingia kwenye njia sahihi ya imani katika Mungu ikiwa watamleta Mungu katika maisha yao halisi, na katika maisha yao ya kawaida ya binadamu. Maneno ya Mungu yanawaongoza ninyi leo; hakuna haja ya ninyi kutafuta na kupapasa kama nyakati zilizopita. Wakati ambapo unaweza kutenda kulingana na maneno ya Mungu, na unaweza kujichunguza na kujitathmini mwenyewe kulingana na hali za binadamu ambazo Nimefichua, basi utaweza kutimiza mabadiliko. Haya siyo mafundisho ya dini, lakini ni kile ambacho Mungu anahitaji kutoka kwa mwanadamu. Leo, hebu Nikuambie jinsi mambo yalivyo: Jishughulishe tu na kutenda kulingana na maneno Yangu. Matakwa Yangu kwako yametegemezwa kwa mahitaji ya mtu wa kawaida. Tayari Nimekwambia maneno Yangu; mradi tu ulenge kuyatenda, utakubaliana na makusudi ya Mungu. Sasa ndio wakati wa kuishi ndani ya maneno ya Mungu. Maneno ya Mungu yameeleza kila kitu, yote yamewekwa wazi, na mradi tu uishi kulingana na maneno ya Mungu, utaishi maisha yaliyo huru kabisa na yaliyokombolewa. Hapo zamani, watu walipomleta Mungu katika maisha yao halisi, walitenda na kupitia mafundisho na kaida nyingi sana za dini; hata katika mambo madogo, wangeomba na kutafuta, wakiweka maneno hayo ya Mungu yaliyosemwa kinaganaga kando na kupuuza kuyasoma. Badala yake, wangeweka juhudi zao zote katika kutafuta—na matokeo yakiwa kwamba hakukuwa na athari. Chukua kwa mfano masuala ya chakula na mavazi: Unaomba na kuyaweka masuala haya mikononi mwa Mungu, ukitaka kwamba Mungu akupangie kila kitu. Mungu anaposikia maneno haya, Atasema: “Je, Napaswa kujishughulisha na mambo madogo kama haya? Ubinadamu wa kawaida na mantiki Niliyokuambia yameenda wapi?” Wakati mwingine, mtu fulani hufanya makosa katika matendo

yake; kisha anaamini kwamba amemkosea Mungu na kisha yeye huanza kujizuia. Hali za watu wengine ni nzuri sana, lakini wanapofanya kitu fulani kidogo kwa njia isiyo sahihi wao huamini kwamba Mungu anawaadibu. Kwa kweli, hayo siyo matendo ya Mungu, lakini ni ushawishi wa akili za watu wenyewe. Wakati mwingine, hakuna kitu kibaya na jinsi unavyopitia tukio, lakini wengine husema kwamba unapitia tukio hilo kwa njia isiyo sahihi, na hivyo unategwa—unakuwa hasi, na mwovu ndani yako. Mara kwa mara, watu wakiwa hasi kwa njia hii, wao huamini kwamba wanaadibiwa na Mungu, lakini Mungu anasema: “Sijafanya kazi yoyote ya kuadibu ndani yako; unawezaje kunilaumu hivyo?” Watu wanakuwa hasi kwa urahisi sana. Wao pia mara kwa mara ni wepesi kuhisi kwa kupindukiana mara nyingi wao hulalamika kuhusu Mungu. Mungu hakutaki wewe uteseke kwa njia hiyo, ilhali wewe unajiruhusu kuingia katika hali hiyo. Hakuna thamani katika kuteseka kwa namna hiyo. Watu hawajui kazi inayofanywa na Mungu, na katika mambo mengi wao ni wajinga na hawawezi kuona vizuri, kwa hiyo wao hunaswa katika dhana na mawazo yao wenyewe, wakiendelea kutegwa kwa kina zaidi. Watu wengine husema kwamba vitu vyote na mambo yote yamo mikononi mwa Mungu—kwa hiyo Mungu hawezi kujua wakati watu wakohasi? Bila shaka Mungu hujua. Unapotegwa katika mawazo ya binadamu, Roho Mtakatifu hana njia ya kufanya kazi ndani yako. Wakati mwingi, watu wengine hutegwa katika hali hasi, lakini Mimi bado huendelea na kazi Yangu. Uwe hasi au chanya, Mimi sizuiliwi na wewe—lakini unapaswa kujua kwamba maneno mengi Ninenayo, na kiasi kikubwa sana cha kazi Nifanyayo, vyote vimeunganika kwa karibu, kimoja kwa kingine, kulingana na hali za watu. Wakati ambapo wewe ni hasi, hili haliizui kazi ya Roho Mtakatifu. Wakati wa kuadibu na majaribu ya kifo, watu wote walitegwa katika hali hasi, lakini hili halikuizuia kazi Yangu. Ulipokuwa hasi, Roho Mtakatifu aliendelea kufanya kilichohitajika kufanywa ndani ya wengine. Unaweza kuacha kufuatilia kwa mwezi mmoja, lakini Mimi naendelea kufanya kazi—chochote ufanyacho katika siku za sasa au za baadaye, hakiwezi kuizuia kazi ya Roho Mtakatifu. Hali nyingine hasi hutokana na udhaifu wa binadamu; wakati ambapo watu wanaamini kwamba hawawezi kweli kutimiza mahitaji ya Mungu au kuyaelewa, wao hugeuka kuwa hasi. Kwa mfano, katika wakati wa kuadibu, maneno ya Mungu yalizungumza kuhusu kumpenda Mungu hadi kwa kiwango fulani katikati ya kuadibu, lakini watu waliamini kwamba hawawezi wenyewe. Walihisi hasa wenye huzuni na wakaomboleza kwamba miili yao ilikuwa imepotoshwa sana na Shetani, na kwamba ubora wao wa tabia ulikuwa duni sana. Walihisi kwamba lilikuwa jambo la kusikitisha sana kuwa walizaliwa katika mazingira haya. Na watu wengine walihisi kwamba wakati ulikuwa umepita sana kwa wao kumwamini Mungu na kumjua Mungu, na kwamba hawakustahili kufanywa wakamilifu. Hizi zote ni hali za kawaida za binadamu.

Mwili wa mwanadamu ni wa Shetani, umejaa tabia za uasi, ni mchafu kiasi cha kusikitisha,

na ni kitu chenye najisi. Watu hutamani raha ya mwili kupita kiasi na kuna maonyesho mengi sana ya mwili; hii ndiyo maana Mungu hudharau mwili wa mwanadamu kwa kiwango fulani. Watu wanapotupa mambo machafu, potovu ya Shetani, wao hupata wokovu wa Mungu. Lakini bado wasipoachana na uchafu na upotovu, basi bado wanamilikiwa na Shetani. Ujanja, udanganyifu, na ukora wa watu yote ni mambo ya Shetani. Wokovu wa Mungu kwako ni ili kukuokoa kutoka katika mambo haya ya Shetani. Kazi ya Mungu haiwezi kuwa na kosa; yote inafanywa ili kuwaokoa watu kutoka gizani. Wakati ambapo umeamini hadi kwa kiwango fulani na unaweza kuachana na upotovu wa mwili, na hufungwi tena pingu na upotovu huu, je, hutakuwa umeokolewa? Wakati ambapo unamilikiwa na Shetani huwezi kumdhihirisha Mungu, wewe ni kitu kichafu, na huwezi kupokea urithi wa Mungu. Mara tu unapotakaswa na kufanywa mkamilifu, utakuwa mtakatifu, utakuwa mtu wa kawaida, na utabarikiwa na Mungu na kuwa mtu anayemfurahisha Mungu. Kazi inayofanywa na Mungu leo ni wokovu, na zaidi ya hayo, ni hukumu, kuadibu, na kulaani. Ina vipengele kadhaa. Nyote mnaona kwamba matamko ya Mungu yana hukumu na kuadibu, na vile vile laana. Nazungumza ili kutimiza athari fulani, kuwafanya watu wajijue, na si kuwafisha watu. Moyo Wangu ni kwa ajili yenu. Kuzungumza ni mbinu mojawapo ambayo Mimi hufanya kazi; kupitia maneno Ninaonyesha tabia ya Mungu na kukuruhusu uelewe mapenzi ya Mungu. Mwili wako waweza kufa, lakini una roho na nafsi. Kama watu wangukuwa na mwili tu, basi hakungekuwa na maana yoyote katika imani yao, wala hakungekuwa na maana yoyote katika kazi hii yote ambayo Nimefanya. Leo, Nazungumza kwa njia moja na kisha nyingine; kwa muda fulani Nawachukia watu mno, na kisha wakati mwingine Mimi ni mwenye upendo wa hali ya juu; Nafanya haya yote kutimiza mabadiliko katika tabia zako, na vile vile kugeuza mawazo yako kuhusu kazi ya Mungu.

Siku za mwisho zimefika na nchi nyingi ulimwenguni ziko katika machafuko. Vurugu ya kisiasa, njaa, ndwele, mafuriko, na ukame unaonekana kila mahali. Kuna maangamizi katika ulimwengu wa mwanadamu; Mbingu pia imetuma msiba hapa chini. Hizi ni ishara za siku za mwisho. Lakini kwa watu, unaonekana kama ulimwengu wa uchangamfu na fahari, ambao unaendelea kuwa hivyo zaidi na zaidi. Mioyo ya watu yote inavutiwa nao, na watu wengi wanaswa na hawawezi kujinasua kutoka kwa ulimwengu; idadi kubwa itadanganywa na wale wanaoshiriki katika hila na uchawi. Usipojitahidi kuendelea mbele, huna maadili, na hujajikita mizizi katika njia ya kweli, utapeperushwa na mawimbi yavumayo ya dhambi. China ni nchi iliyo nyuma zaidi kimaendeleo kuliko zote; ni nchi ambapo joka kuu jekundu hulala likiwa limejiviringisha, ina watu wengi zaidi wanaoabudu sanamu na kushiriki katika uchawi, ina hekalu nyingi zaidi, na ni mahali ambapo pepo wachafu huishi. Ulizaliwa kutoka kwayo, umeelimishwa nayo na ukaloweshwa katika ushawishi wake; umepotoshwa na kuteswa nayo, lakini baada ya kugutushwa unaachana nayo na unapatwa kabisa na Mungu. Huu ni utukufu wa

Mungu, na hii ndiyo maana hatua hii ya kazi ina umuhimu mkubwa. Mungu amefanya kazi ya kiwango kikubwa hivi, amenena maneno mengi sana, na hatimaye Atawapata ninyi kabisa—hii ni sehemu moja ya kazi ya usimamizi ya Mungu, na ninyi ndio “mateka wa ushindi” wa vita vya Mungu na Shetani. Kadiri mnavyozidi kuelewa ukweli na kadiri maisha yenu ya kanisa yalivyo bora zaidi, ndivyo joka kuu jekundu linavyotishwa zaidi. Haya yote ni mambo ya ulimwengu wa kiroho—ni vita vya ulimwengu wa kiroho, na Mungu anapokuwa mshindi, Shetani ataaibishwa na kuanguka chini. Hatua hii ya kazi ya Mungu ina umuhimu wa ajabu. Mungu anafanya kazi kwa kiwango kikubwa sana na kukiokoa kabisa kikundi hiki cha watu ili uweze kuponyoka kutoka kwa ushawishi wa Shetani, uishi katika nchi takatifu, uishi katika nuru ya Mungu, na uwe na uongozi na mwongozo wa nuru. Kisha kuna maana katika maisha yako. Mnachokula na kuvaa ni tofauti na wasioamini; mnafurahia maneno ya Mungu na kuishi maisha yenye maana—na wao hufurahia nini? Wao hufurahia tu “urithi wa babu” zao na “fahari yao ya kitaifa.” Hawana hata chembe ndogo kabisa ya ubinadamu! Mavazi, maneno, na matendo yenu yote ni tofauti na yao. Hatimaye, mtatoroka kabisa kutoka katika uchafu, msitegwe tena katika majaribu ya Shetani, na mpate riziki ya Mungu ya kila siku. Mnapaswa kila mara kuwa waangalifu. Ingawa mnaishi mahali pachafu hamjawekwa mawaa na uchafu na mnaweza kuishi ubavuni mwa Mungu, mkipokea ulinzi Wake mkuu. Mungu amewachagua kutoka miongoni mwa wote walio katika nchi hii ya manjano. Je, ninyi sio watu waliobarikiwa zaidi? Wewe ni kiumbe aliyeumbwa—unapaswa bila shaka kumwabudu Mungu na kufuatilia maisha yenye maana. Usipomwabudu Mungu lakini unaishi ndani ya mwili wako mchafu, basi wewe si mnyama tu aliye ndani ya vazi la mwanadamu? Kwa kuwa wewe ni binadamu, unapaswa kujitumia kwa ajili ya Mungu na kuvumilia kila mateso! Unapaswa kukubali kwa furaha na kwa hakika mateso kidogo unayopitia leo na kuishi maisha yenye maana, kama Ayubu na Petro. Katika ulimwengu huu, mwanadamu huvaa mavazi ya ibilisi, hula chakula kutoka kwa ibilisi, na hufanya kazi na kutumika chini ya uelekezi wa Shetani, na kukanyagiwa kabisa ndani ya uchafu wake. Usipoelewa maana ya maisha au kupata njia ya kweli, basi kuna umuhimu gani katika kuishi kwa namna hii? Ninyi ni watu mnaofuatilia njia sahihi, wale mnaotafuta maendeleo. Ninyi ni watu ambao huinuka katika nchi ya joka kuu jekundu, wale ambao Mungu huwaita wenye haki. Je, hayo si maisha yenye maana zaidi?

Fumbo la Kupata Mwili (1)

Katika Enzi ya Neema, Yohana alimwandalia Yesu njia. Hangeweza kufanya kazi ya Mungu Mwenyewe ila alitimiza tu kazi ya mwanadamu. Ingawa Yohana alikuwa mtangulizi wa Bwana; hangeweza kumwakilisha Mungu; alikuwa tu binadamu aliyetumiwa na Roho Mtakatifu. Kufuatia ubatizo wa Yesu, “Roho Mtakatifu alimshukia Yeye kwa mfano wa njiwa.” Kisha Akaanza kazi Yake, hivyo, Alianza kufanya huduma ya Kristo. Hiyo ndiyo maana Alichukua

utambulisho wa Mungu, kwa sababu Alitoka Kwa Mungu. Haijalishi jinsi imani Yake ilivyokuwa kabla ya hii—labda wakati mwingine ilikuwa dhaifu, au wakati mwingine ilikuwa na nguvu—hayo ndiyo yalikuwa maisha Yake ya kawaida ya binadamu kabla Afanye huduma Yake. Baada ya kubatizwa (kuteuliwa), mara moja Alikuwa na nguvu na utukufu wa Mungu pamoja Naye, na hivyo Akaanza Kufanya huduma Yake. Angetenda ishara na maajabu, Atende miujiza, Alikuwa na nguvu na mamlaka, kwani Alifanya kazi kwa niaba ya Mungu Mwenyewe; Alifanya kazi ya Roho badala Yake na kuonyesha sauti ya Roho Mtakatifu; kwa hivyo Alikuwa Mungu Mwenyewe. Hili halina pingamizi. Yohana alitumiwa na Roho Mtakatifu. Hangemwakilisha Mungu, na hakungekuwa na uwezekano wa yeye kumwakilisha Mungu. Kama angetaka kufanya hivyo, Roho Mtakatifu hangelikubali, kwani hangeweza kufanya kazi ambayo Mungu Mwenyewe alinuia kukamilisha. Labda kulikuwa na mengi ndani yake yaliyokuwa ya mapenzi ya mwanadamu, ama kitu kilichokuwa cha mwacha maadili; hakuna hali yoyote ambapo angemwakilisha Mungu moja kwa moja. Makosa Yake na mambo yasiyo sahihi yalimwakilisha yeye pekee, lakini kazi Yake ilikuwa uwakilishi wa Roho Mtakatifu. Ilhali, huwezi kusema kuwa yeye mzima alimwakilisha Mungu. Je upotovu na kuwa kwake na makosa kungemwakilisha Mungu pia? Kuwa na makosa katika kumwakilisha mwanadamu ni kawaida, lakini kama alikuwa na upotovu katika kumwakilisha Mungu, basi si hiyo ingekuwa kutomheshimu Mungu? Je hilo halingekuwa kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu? Roho Mtakatifu hawezi kumruhusu mwanadamu asimame mahali pa Mungu anavyotaka, hata kama anasifiwa na wengine. Kama yeye si Mungu, basi hataweza kubaki akiwa amesimama mwishowe. Roho Mtakatifu hamkubali mwanadamu amwakilishe Mungu vile mwanadamu atakavyo! Kwa mfano, Roho Mtakatifu alimshuhudia Yohana na pia kumtambulisha kuwa mmoja wa wale watakaomwandalia Yesu njia, lakini kazi iliyofanywa ndani Yake na Roho Mtakatifu ilikuwa imepimwa vizuri. Kilichotakiwa kwa Yohana ilikuwa awe wa kutayarisha njia ya Yesu tu, kumtayarishia Yesu njia. Hiyo ni kusema, Roho Mtakatifu Aliiunga mkono kazi yake katika kutengeneza njia na kumruhusu afanye kazi ya aina hiyo pekee, hakuna mwingine. Yohana alimwakilisha Eliya, na alimwakilisha nabii aliyetengeneza njia. Hili liliungwa mkono na Roho Mtakatifu; bora kazi yake iwe kutengeneza njia, Roho Mtakatifu aliiunga mkono. Hata hivyo, kama angeweka madai kwamba yeye ni Mungu Mwenyewe na amekuja kumaliza kazi ya ukombozi, Roho Mtakatifu lazima amwadhibu. Haijalishi ukuu wa kazi ya Yohana, na ingawa iliungwa mkono na Roho Mtakatifu, kazi Yake ilibaki katika mipaka. Ni ukweli hakika kuwa kazi yake iliungwa mkono na Roho Mtakatifu, lakini nguvu aliyopewa katika wakati huo iliwekewa mipaka tu katika kutengeneza njia. Hangeweza, hata kidogo, kufanya kazi nyingine, kwani alikuwa tu Yohana aliyetengeneza njia, ila si Yesu. Kwa hivyo ushuhuda wa Roho Mtakatifu ni muhimu, lakini kazi ambayo mwanadamu anaruhusiwa kufanya na Roho Mtakatifu ni muhimu zaidi. Je, Yohana hakushuhudiwa sana? Kazi yake haikuwa kuu pia? Lakini kazi

aliyofanya haingeshinda ile ya Yesu, kwani alikuwa mwanadamu tu aliyetumiwa na Roho Mtakatifu na hangeweza kumwakilisha Mungu moja kwa moja, na kwa hiyo kazi aliyofanya ilikuwa yenye mipaka. Baada ya yeye kuimaliza kazi ya kuandaa njia, Roho Mtakatifu hakuthibitisha ushuhuda wake tena, hakuna kazi mpya iliyomfuata yeye tena, na aliondoka kazi ya Mungu Mwenyewe ilipoanza.

Kuna wengine ambao wamepagawa na roho wachafu na wanalia kwa kusesitiza wakisema, “Mimi ni Mungu!” Lakini mwishowe, hufichuliwa, kwani wanafanya kazi kwa niaba ya kiumbe asiyefaa. Wanawakilisha Shetani na Roho Mtakatifu hajali kuwahusu hata kidogo. Hata ujiinue vipi, ama kwa nguvu kiviipi, wewe bado ni kiumbe aliyeumbwa na wewe unamilikiwa na Shetani. Mimi sipigi mayowe Nikisema, “Mimi ni Mungu, Mimi ni Mwana Mpendwa wa Mungu!” Lakini kazi Nifanyayo ni ya Mungu. Kuna haja Nipige mayowe? Hakuna haja ya kujiinua. Mungu hufanya kazi Yake Mwenyewe na hahitaji mwanadamu kumpa ruhusa ama cheo kubwa, na kazi Yake inatosha kuwakilisha utambulisho Wake na cheo. Kabla ya ubatizo Wake, si Yesu alikuwa Mungu Mwenyewe? Je, Yeye hakuwa mwili wa Mungu? Hakika haiwezi kusemekana kuwa Alikuwa Mwana wa pekee wa Mungu baada ya kushuhudiwa? Je, hakukuwa na mwanadamu jina lake Yesu kitambo kabla Aanze kazi Yake? Huwezi kuleta njia mpya ama kumwakilisha Roho. Huwezi kueleza kazi ya Roho ama maneno Anenayo. Huwezi kufanya kazi ya Mungu Mwenyewe ama ile ya Roho. Huwezi kuelezea hekima, ajabu na mambo ya Mungu yasiyoeleweka, ama tabia yote ambayo Mungu humwadibu mwanadamu kupitia kwayo. Kwa hivyo madai yako ya kila mara ya kusema kuwa wewe ni Mungu hayajalishi; unalo tu jina lakini huna dutu. Mungu Mwenyewe Amekuja, lakini hakuna anayemtambua, ilhali Anaendelea na kazi Yake na Anafanya hivyo kwa uwakilishi wa Roho. Haijalishi unamwita mwanadamu ama Mungu, Bwana ama Kristo, ama umwite dada, yote ni sawa. Lakini kazi Afanyayo ni ile ya Roho na Anawakilisha kazi ya Mungu Mwenyewe. Hajali ni jina gani mwanadamu anamwita. Je, jina hilo linaweza kuamua kazi Yake? Bila kujali unachomwita, kutoka kwa mtazamo wa Mungu, Yeye ni kupata mwili kwa Roho wa Mungu; Anawakilisha Roho na amekubaliwa na Yeye. Huwezi kutengeneza njia ya enzi mpya, na huwezi kuhitimisha enzi nzee na huwezi kukaribisha enzi mpya ama kufanya kazi mpya. Kwa hivyo, huwezi kuitwa Mungu!

Hata mwanadamu anayetumiwa na Roho Mtakatifu hawezi kumwakilisha Mungu Mwenyewe. Na mwanadamu huyu hawezi tu kumwakilisha Mungu bali pia kazi yake haiwezi kumwakilisha Mungu moja kwa moja. Hivyo ni kusema uzoefu wa mwanadamu hauwezi kuwekwa moja kwa moja katika usimamizi wa Mungu, na hauwezi kuwakilisha usimamizi wa Mungu. Kazi yote ambayo Mungu Mwenyewe hufanya ni kazi Anayolenga Kufanya katika mpango Wake wa usimamizi na inahusiana na usimamizi mkuu. Kazi ifanywayo na mwanadamu (mwanadamu anayetumiwa na Roho Mtakatifu) hukidhi uzoefu wake binafsi. Anapata njia mpya

ya uzoefu mbali na ile iliyotembelewa na wale waliomtangulia na anawaongoza ndugu zake chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Kinachotolewa na watu hawa ni uzoefu wao ama maandishi ya kiroho ya watu wa kiroho. Ingawa wanatumiwa na Roho Mtakatifu, kazi ya watu kama hao haina uhusiano na kazi ya usimamizi mkuu katika mpango wa miaka elfu sita. Wamesimamishwa na Roho Mtakatifu katika wakati tofauti kuongoza watu katika mkondo wa Roho Mtakatifu hadi wakamilishe kazi yao ama maisha yao yafike mwisho. Kazi wanayofanya ni kutayarisha njia ifaayo kwa ajili ya Mungu Mwenyewe ama kuendeleza kitu kimoja kwa usimamizi wa Mungu Mwenyewe katika dunia. Watu hao hawawezi kufanya kazi kuu katika usimamizi Wake, na hawawezi kufungua njia mpya, ama kumaliza kazi yote ya Mungu kutoka enzi ya kitambo. Kwa hivyo, kazi wafanyayo inawakilisha kiumbe aliyeumbwa pekee akifanya kazi Yake na hawezi kuwakilisha Mungu Mwenyewe Akifanya huduma Yake. Hii ni kwa sababu kazi wanayofanya haifanani na ile inayofanywa na Mungu Mwenyewe. Kazi ya kukaribisha enzi mpya haiwezi kufanywa na mwanadamu kwa niaba ya Mungu. Haiwezi kufanywa na mwingine ila Mungu Mwenyewe. Kazi yote inayofanywa na mwanadamu ni kufanya wajibu wake kama mmoja wa viumbe na inafanywa akiguswa au kupewa nuru na Roho Mtakatifu. Uongozi ambao watu hao hupeana ni jinsi ya kuzoea katika kila siku ya maisha ya mwanadamu na jinsi mwanadamu anapaswa kutenda kwa maelewano na mapenzi ya Mungu. Kazi ya mwanadamu haihusishi usimamizi wa Mungu ama kuwakilisha kazi ya Roho. Kama mfano, kazi ya Witness Lee na Watchman Nee ilikuwa ni kuongoza njia. Njia iwe mpya au nzee, kazi ilifanywa kwa misingi ya kanuni ya kutozidi Biblia. Haijalishi kama makanisa ya mitaa yalirejeshwa yalivyokuwa awali au yalijengwa, kazi yao ilikuwa ni kuanzisha makanisa. Kazi waliyofanya iliendeleza kazi ambayo Yesu Kristo na mitume Wake walikuwa hawajamaliza au kuendeleza zaidi kwenye Enzi ya Neema. Kile walichofanya katika kazi yao kilikuwa ni kurejesha kile ambacho Yesu Kristo Alikuwa Ameomba katika kazi Yake ya vizazi vitakavyokuja baada Yake Yeye, kama vile kuhakikisha kwamba vichwa vyao vimefunikwa, ubatizo, umegaji mkate, au unywaji wa mvinyo. Inaweza kusemekana kwamba kazi yao ilikuwa kubakia tu kwenye Biblia na kutafuta njia zinazotokana tu na Biblia. Hawakupiga hatua yoyote mpya kamwe. Hivyo basi, mtu anaweza kuona tu ugunduzi wa njia mpya ndani ya Biblia, pamoja na mazoea bora zaidi na yenye uhalisia zaidi. Lakini mtu hawezi kupata katika kazi yao mapenzi ya sasa ya Mungu, isitoshe hawezi kupata kazi mpya ambayo Mungu Atafanya kwenye siku za mwisho. Hii ni kwa sababu njia ambayo walitembelea ilikuwa bado ile nzee; hakukuwa na maendeleo yoyote na kitu chochote kipya. Waliendelea kuufuata ukweli wa “kule kusulubishwa kwa Yesu,” mazoea ya “kuwaomba watu kutubu na kukiri dhambi zao,” msemu kwamba “yule atakayevumilia hata mwisho ataokoka,” na msemu kwamba “mwanamume ndiye kichwa cha mwanamke, na mwanamke lazima amtii mume wake.” Aidha, waliendeleza dhana ya kitamaduni kwamba “akina dada hawawezi kuhubiri, na wanaweza tu kutii.” Ikiwa njia kama hiyo ya uongozi

ingeendelea, basi Roho Mtakatifu asingewahi kuweza kutekeleza kazi mpya, kuwaweka binadamu huru kutokana na mafundisho, au kuwaongoza binadamu kwenye himaya ya uhuru na urembo. Hivyo basi, hatua hii ya kazi ya mabadiliko ya enzi lazima ifanywe na kuzungumzwa na Mungu Mwenyewe, la sivyo hakuna mwanadamu anayeweza kufanya hivyo badala Yake. Mpaka hapa, kazi yote ya Roho Mtakatifu iliyo nje ya mfululizo huu imesimama, na wale waliotumiwa na Roho Mtakatifu wamepoteza mwelekeo wao. Kwa hivyo, kwa sababu kazi ya wanadamu wanaotumiwa na Roho Mtakatifu si sawa na kazi ifanywayo na Mungu Mwenyewe, utambulisho wao na wanayefanya kazi kwa niaba yake ni tofauti. Hii ni kwa sababu kazi ambayo Roho Mtakatifu Analenga Kufanya ni tofauti, na hapo kutoa utambulisho tofauti na hadhi kwa wale wote wafanyao kazi. Wanadamu wanaotumiwa na Roho Mtakatifu wanaweza kufanya kazi mpya na wanaweza kutoa kazi iliyofanywa katika enzi iliyopita, lakini kazi yao haiwezi kueleza tabia na mapenzi ya Mungu kwa enzi mpya. Wanafanya kazi ili kuondoa kazi ya enzi iliyopita tu, sio kufanya kazi mpya kuwakilisha moja kwa moja tabia ya Mungu Mwenyewe. Hivyo, haijalishi matendo mangapi yaliyopitwa na wakati wanakomesha ama matendo mapya wanaanzisha, bado wanawakilisha mwanadamu na viumbe vilivyoundwa. Mungu Mwenyewe Akifanya kazi, hata hivyo, Hatangazi wazi kukomeshwa kwa matendo ya enzi ya zamani au kutangaza moja kwa moja kuanzishwa kwa enzi mpya. Yeye hufanya kazi Yake moja kwa moja na kwa njia ya moja kwa moja. Yeye hufanya kazi Anayolenga kufanya moja kwa moja; hivyo, yeye hueleza moja kwa moja kazi Aliyoleta, Anafanya kazi Yake moja kwa moja Alivyolenga hapo awali, Akieleza uwepo Wake na tabia Yake. Mwanadamu anavyoona, tabia Yake na kazi Yake pia hazifanani na zile ya kitambo. Hata hivyo, kutoka kwa mtazamo wa Mungu Mwenyewe, huku ni kuendelea na ujenzi zaidi wa kazi Yake. Mungu Mwenyewe Akifanya kazi, Anaeleza neno Lake na Analeta kazi mpya moja kwa moja. Tofauti ni, mwanadamu akifanya kazi, ni kwa ukombozi na kusoma, ama ni kwa maendeleo ya maarifa na mpangilio wa mazoezi iliyojengwa juu ya msingi wa kazi za wengine. Hiyo ni kusema, umuhimu wa kazi inayofanywa na mwanadamu ni ya kuweka mkataba na “kutembea njia za kitambo kwa vitu mpya.” Hii inamanisha kuwa hata njia ambayo inatembelwa na watu wanaotumiwa na Roho Mtakatifu imejengwa juu ya yale yalifunguliwa na Mungu Mwenyewe. Kwa hivyo mwanadamu ni baada ya yote mwanadamu, na Mungu ni Mungu.

Yohana alizaliwa kwa ahadi, kama vile Isaka alivyoza kwa Abrahamu. Alimwandalia Yesu njia na alifanya kazi nyingi, lakini hakuwa Mungu. Badala yake, anafikiriwa kuwa ni nabii kwa sababu alimwandalia tu Yesu njia. Kazi yake ilikuwa kuu pia, na ni baada ya yeye kuandaa njia tu ndipo Yesu akaanza kazi Yake kwa urasimu. Kimsingi, yeye alimfanyia tu Yesu kazi, na kazi yake ilikuwa katika huduma ya kazi ya Yesu. Baada ya yeye kuiandaa njia, Yesu akaanza kazi Yake, kazi iliyokuwa mpya zaidi, dhahiri zaidi, na katika utondoti mkubwa zaidi. Yohana

alifanya tu kazi ya mwanzo; nyingi ya kazi mpya ilifanywa na Yesu. Yohana alifanya kazi mpya pia, lakini sio yeye aliyeianzisha enzi mpya. Yohana alizaliwa kwa ahadi, na jina lake kupewa na malaika. Katika wakati huo wengine walitaka kumpa jina la baba yake Zakaria, lakini mama yake alinena akisema, “Mtoto huyu hawezi kuitwa kwa jina hilo. Anapaswa kuitwa Yohana.” Haya yote yalielekezwa na Roho Mtakatifu. Jina la Yesu pia lilikuwa limeelekezwa na Roho Mtakatifu, na Alizaliwa wa Roho Mtakatifu, na kwa ahadi ya Roho Mtakatifu. Yesu Alikuwa Mungu, Kristo, na Mwana wa mtu. Kazi ya Yohana ilikuwa kuu pia, lakini mbona hakuitwa Mungu? Ni nini tofauti kati ya kazi iliyofanywa na Yesu na ile iliyofanywa na Yohana? Je, sababu pekee ni kwa kuwa Yohana ndiye aliyetengeneza njia ya Yesu? Au ni kwa sababu ilikuwa imepangwa na Mungu? Ingawa Yohana alisema kuwa, “Ninyi tubuni: kwa kuwa ufalme wa mbinguni uko karibu,” na kuhubiri pia injili ya ufalme wa mbinguni, kazi yake haikuwa yenye kina na ilijumuisha tu mwanzo. Kinyume, Yesu Alikaribisha enzi mpya na kuikamilisha enzi ya kitambo, lakini pia Alitimiza sheria ya Agano la Kale pia. Kazi Aliyofanya ni kubwa kuliko ile ya Yohana, na Alikuwa kuwakomboa wanadamu wote—Alifanya hatua hii ya kazi. Yohana alitayarisha tu njia. Ingawa kazi yake ilikuwa kubwa, maneno yake mengi, na wale wafuasi waliomfuata wengi, kazi yake haikufanya kitu kingine ila kuletea mwanadamu mwanzo mpya. Mwanadamu hakupokea maisha, njia, ama ukweli wa ndani kutoka kwake, wala mwanadamu hakupata kupitia kwake ufahamu wa mapenzi ya Mungu. Yohana alikuwa nabii mkuu (Eliya) aliyeanza msingi mpya wa kazi ya Yesu na kutayarisha aliyeteuliwa; alikuwa mtangulizi wa Enzi ya Neema. Mambo kama haya hayawezi kutambuliwa kirahisi kwa kuchunguza kuonekana kwao kwa kawaida. Hasa sana, Yohana alifanya kazi kubwa; zaidi ya hayo, alizaliwa kutoka kwa ahadi ya Roho Mtakatifu, na kazi yake ikashikiliwa na Roho Mtakatifu. Hivyo, kutofautisha kati ya utambulisho wao inaweza kufanywa tu kupitia kazi yao, kwa kuwa sura tu ya nje ya mwanadamu haiwezi kuonyesha dutu yake, na mwanadamu hawezi kuhakikisha ushuhuda wa kweli wa Roho Mtakatifu. Kazi iliyofanywa na Yohana na ile iliyofanywa na Yesu si sawa na ilikuwa ya asili tofauti. Hii ndiyo inafaa kuonyesha kama yeye ni Mungu ama sio Mungu. Kazi ya Yesu ilikuwa kuanza, kuendelea, kuhitimisha na kukamilisha. Kila moja ya hatua hizi zilichukuliwa na Yesu, ilhali kazi ya Yohana haikuwa zaidi ya kuanzisha. Hapo mwanzo, Yesu Alieneza injili na kuhubiri njia ya kutubu, na Akaendelea mpaka kumbatiza mwanadamu, kuponya magonjwa, na kukemea mapepo. Mwishowe, Alimkomboa mwanadamu kutoka kwa dhambi na kukamilisha kazi Yake ya enzi yote. Alimhubiria mwanadamu na kueneza injili ya ufalme wa mbinguni katika sehemu zote. Hii ilikuwa sawa na Yohana, tofauti ikiwa kwamba Yesu Alikaribisha enzi mpya na kuleta Enzi ya Neema kwa mwanadamu. Kutoka kwa Mdomo Wake lilitoka neno jinsi mwanadamu anavyopaswa kutenda na njia mwanadamu anayopaswa kufuata Enzi ya Neema, na mwishowe, Akamaliza kazi ya Wokovu. Kazi kama hiyo haingeweza kutekelezwa na Yohana. Kwa hivyo, ni Yesu ndiye

Aliyefanya Kazi Ya Mungu Mwenyewe, na ni Yeye ndiye Mungu Mwenyewe na Anamwakilisha Mungu moja kwa moja. Dhana za mwanadamu zinasema kwamba wale wote waliozaliwa kwa ahadi, waliozaliwa kwa Roho, waliothibitishwa na Roho Mtakatifu, na waliozifungua njia mpya ni Mungu. Kwa kadri ya fikira hii, Yohana pia angekuwa Mungu, na Musa, Abrahamu, na Daudi..., wao pia wangukuwa Mungu. Je, huu sio mzaha mkubwa?

Kabla ya kutekeleza huduma Yake, Yesu pia alikuwa mtu wa kawaida tu Aliyefuata kazi yoyote ile ya Roho Mtakatifu. Haijalishi kama Alifahamu utambulisho Wake mwenyewe wakati huo, Alitii yote yaliyotoka kwa Mungu. Roho Mtakatifu hakufichua kamwe utambulisho Wake kabla ya kuanza kwa huduma Yake. Ni baada ya Yeye kuanza huduma Yake ndipo Alitangua amri hizo na sheria hizo, na ni baada tu ya Yeye kuanza kwa urasimu kutekeleza huduma Yake ndipo maneno Yake yakajaa mamlaka na nguvu. Ni baada tu ya kuanza huduma Yake ndipo kazi Yake ya kuleta enzi mpya ilianza. Kabla ya hili, Roho Mtakatifu aliendelea kujificha ndani Yake kwa miaka 29, wakati ambapo Alimwakilisha mwanadamu tu na hakuwa na utambulisho wa Mungu. Kazi ya Mungu ilianza na Yeye kufanya kazi na kutekeleza huduma Yake, Aliifanya kazi Yake kama ilivyopangwa ndani, bila kujali mwanadamu alijua kiasi gani kumhusu, na kazi Yake ilikuwa uwakilishi wa moja kwa moja wa Mungu Mwenyewe. Wakati huo, Yesu aliwauliza waliokuwa karibu na Yeye, “Mnasema Mimi ni nani?” Nao wakajibu, “Wewe ni mkuu zaidi kati ya manabii na tabibu wetu mwema.” Na wengine wakajibu, “Wewe ni kuhani mkuu wetu.” ... Majibu mbalimbali yalitolewa; wengine walisema kwamba Alikuwa Yohana, kwamba Alikuwa Eliya. Kisha Yesu akamgeukia Simoni Petro na kuuliza, “Wewe unasema Mimi ni nani?” Petro akajibu, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aishiye.” Tangu wakati huo kuendelea watu wakafahamu kwamba Yeye alikuwa Mungu. Hili lilipofahamishwa, ni Petro ndiye aliyekuwa wa kwanza kupata utambuzi huu na kutoka kinywani mwake hayo yalisemwa. Kisha Yesu akanena, “Ulichosema hakikufichuliwa na mwili na damu, bali na Baba Yangu.” Baada ya ubatizo Wake, kama ilijulikana kwa wengine au la, kazi Yake ilikuwa kwa niaba ya Mungu. Alikuwa kutekeleza kazi Yake, sio kufichua utambulisho Wake. Ni baada tu ya maneno hayo kusemwa na Petro ndipo utambulisho Wake ukajulikana na mwanadamu kwa dhahiri. Kama ulifahamu kwamba Alikuwa Mungu Mwenyewe au la, Alianza kazi Yake wakati ambapo muda ulifika. Aliendelea na kazi Yake kama ulifahamu au la. Hata kama ungeikana, Angeitekeleza kazi Yake na angeimaliza ulipokuwa wakati wa kufanya hivyo. Alikuwa kufanya kazi na kutekeleza huduma Yake, sio kwa mwanadamu kuujua mwili Wake, bali kwa mwanadamu kuipokea kazi Yake. Iwapo hutambui kwamba hatua ya kazi siku hii ni ile ya Mungu Mwenyewe, ni kwa sababu huna maono. Hata hivyo, huwezi kukataa hatua hii ya kazi; kukosa kwako kuitambua hakumaanishi kuwa Roho Mtakatifu hafanyi kazi ama ya kwamba kazi Yake si sawa. Wengine hata hulinganisha kazi ya wakati huu dhidi ya ile ya Yesu katika Biblia,

na kutumia tofauti zilizopo kati ya kazi hizi kukataa hatua hii ya kazi. Je haya si matendo ya aliyepofushwa? Yote yaliyoandikwa katika Biblia ni machache na hayawezi kuwakilisha kazi yote ya Mungu. Injili Nne zina chini ya sura mia moja zote pamoja ambamo mliandikwa mambo yale yaliotendeka yanayohesabika, kwa mfano Yesu Akilaani mti wa mkuyu, Petro akimkana Bwana mara tatu, Yesu Akiwaonekania wanafunzi Wake baada ya kusulubiwa na ufufuo Wake, Akifunza kuhusu kufunga, kufunza kuhusu maombi, kufunza kuhusu talaka, kuzaliwa na kizazi cha Yesu, uteuzi wa Yesu wa wanafunzi, na mengine mengi. Hata hivyo, mwanadamu anayathamini kama hazina, hata kuthibitisha kazi ya leo kulingana nayo. Hata wanaamini kuwa Yesu Alitenda kiasi tu katika muda baada ya kuzaliwa Kwake. Ni kana kwamba wanaamini kuwa Mungu anaweza kufanya hayo tu, kwamba hakuna kazi nyingine. Je huu si upumbavu?

Kipindi ambacho Yesu alikuwa nacho duniani kilikuwa miaka thelathini na mitatu na nusu, yaani, Aliishi duniani miaka thelathini na mitatu na nusu. Ni miaka mitatu na nusu pekee ya kipindi hiki ndiyo iliyotumiwa kutekeleza huduma Yake, na, ile iliyobaki, Aliishi tu maisha ya binadamu ya kawaida. Hapo mwanzo, Alihudhuria ibada katika sinagogi na hapo Alisikiliza mahubiri ya makuhani, na ujumbe wa wengine; Alipata ufahamu mwingi wa Biblia. Hakuzaliwa na ufahamu kama huo, na aliupata tu kupitia kusoma na kusikiliza. Imerekodiwa kwa dhahiri ndani ya Biblia kwamba Aliwauliza waalimu maswali ndani ya sinagogi alipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili: Unabii wa manabii wa zamani ulikuwa upi? Na kuhusu sheria za Musa? Maandiko? Na kuhusu mwanadamu kumhudumia Mungu katika mavazi ya kikuhani ndani ya hekalu? ... Aliuliza maswali mengi, kwani Hakuwa na maarifa au ufahamu. Ingawa mimba Yake ilitungwa na Roho Mtakatifu, Alizaliwa kama mwanadamu wa kawaida kamili. Licha ya sifa nyingine maalumu, Yeye hata hivyo alikuwa mwanadamu wa kawaida. Hekima Yake ilikua kwa kuendelea kwa kukubaliana na kimo na umri Wake, na maisha Yake yaliendelea kama yale ya mwanadamu wa kawaida. Katika mawazo ya mwanadamu, Yesu hakupitia utoto na wala ujana; mwanadamu ana fikira kwamba Alizaliwa katika maisha ya mwanadamu mwenye umri wa miaka thelathini na mitatu, na Akasulubiwa baada ya kuimaliza kazi Yake. Wao huamini kwamba labda maisha Yake hayakupitia maendeleo kama ya mwanadamu wa kawaida; labda Hakula wala kushirikiana na mwanadamu, na Hakutazamwa kwa urahisi na mwanadamu. Labda Alikuwa mkengeuko ambaye angewatisha wale waliomwona Yeye, kwani Yeye ni Mungu. Watu huamini kuwa Mungu mwenye Mwili lakini haishi jinsi mwanadamu wa kawaida anavyoishi; wanaamini kuwa ni msafi hata hawezi kusugua meno Yake ama kuosha uso Wake, kwani ni mtu mtakatifu. Je hizi kikamilifu si dhana ya mwanadamu? Biblia haina rekodi yoyote kuhusu maisha ya Yesu kama mwanadamu, kazi Yake pekee, lakini hili halithibitishi kuwa hakuwa na ubinadamu wa kawaida ama hakuishi maisha ya mwanadamu wa kawaida kabla ya umri wa miaka thelathini. Alianza kazi Yake rasmi Akiwa na miaka 29, lakini huwezi kukana maisha

Yake yote kama mwanadamu kabla ya umri huo. Biblia iliacha hatua hiyo katika maandishi Yake; kwani yalikuwa maisha Yake kama mwanadamu wa kawaida na si hatua ya kazi Yake takatifu, hakukuwa na haja ya maneno hayo kuandikwa chini. Kwani kabla ya ubatizo wa Yesu, Roho Mtakatifu hakufanya kazi Yake moja kwa moja, lakini akadumisha maisha Yake kama mwanadamu wa kawaida tu hadi siku ambayo Yesu Alikuwa Anapaswa kuanza huduma Yake. Ingawa Alikuwa Mungu katika mwili, Alipitia mchakato wa kukomaa kama jinsi mwanadamu wa kawaida afanyavyo. Hatua hii iliwachwa nje ya Biblia, kwani haingeleta usaidizi mkubwa kwa kukuwa kwa maisha ya mwanadamu. Kabla ya ubatizo Wake ulikuwa wakati ambapo hakujulikana, na wala Hakutenda ishara na miujiza. Baada tu ya ubatizo wa Yesu ndipo Alipoanza kazi ya ukombozi wa mwanadamu, kazi ambayo imejaa sana neema, ukweli, na upendo na huruma. Mwanzo wa kazi hii ndio ulikuwa pia mwanzo wa Enzi ya Neema; kwa sababu hii, matukio haya yaliandikwa chini na kupitishwa kwa vizazi mpaka wakati huu. Ilifungua njia na kuyafanya yote kupata mafanikio kwa wale walio katika Enzi ya Neema kuitembea njia ya enzi hiyo na kuitembea njia ya msalaba. Ingawa rekodi za hayo ziliandikwa na mwanadamu, zote ni maelezo ya ukweli, zenye makosa madogo tu katika mambo fulani. Hata hivyo, mtu hawezi kukana ukweli wa mambo hayo. Hayo yote ni ya ukweli, ingawa makosa yalionekana yalipoandikwa na mwanadamu. Kuna wengine atakaosema kwamba, kama Yesu alikuwa sawa na binadamu kawaida, kwa hiyo ingekuwaje kwamba Alikuwa mwenye uwezo wa kufanya ishara na maajabu? Siku arobaini za majaribu ambayo Yesu alipitia ni ishara ya muujiza, ambayo mwanadamu wa kawaida hangekuwa na uwezo wa kutimiza. Siku Zake arobaini za majaribu ilikuwa kazi ya Roho Mtakatifu; basi ni vipi ambavyo mtu anaweza kusema kwamba hakuna ya rohoni hata kidogo ndani Yake? Kufanya Kwake ishara na maajabu hakuonyeshi kwamba Hakuwa mwanadamu wa kawaida bali mwanadamu anayezidi uwezo wa binadamu; ni kwamba tu Roho Mtakatifu alifanya kazi ndani ya mwanadamu wa kawaida kama Yeye, na hivyo kumwezesha Yeye kutekeleza miujiza na kufanya kazi kuu zaidi. Kabla ya Yesu kufanya huduma Yake, ama isemwavyo katika Biblia, kabla ya Roho Mtakatifu kushuka juu Yake, Yesu Alikuwa mwanadamu wa kawaida na bila kuwa na chochote kisicho cha kawaida. Roho Mtakatifu Aliposhuka, hiyo ni, Alipoanza kazi ya huduma Yake, Alijazwa na vitu vya kimiujiza. Kwa njia hii, mwanadamu anaanza kuamini kwamba mwili wa Mungu hauna ubinadamu wa kawaida; aidha anafikiri kimakosa kwamba Mungu mwenye mwili ana uungu tu, sio ubinadamu. Hakika, Mungu akujapo duniani kufanya kazi Yake, yote aonayo mwanadamu ni matukio yasiyo ya kawaida. Chote anachoona kwa macho yake na anachosikia kwa masikio yake si cha kawaida, kwani kazi Yake na maneno Yake hayaeleweki na kufikiwa naye. Kitu cha mbinguni kikiletwa duniani, itakuwa vipi kiwe kitu cha kawaida? Mafumbo ya ufalme wa mbinguni yanapoletwa duniani, mafumbo yasiyoweza kufikiriwa na kueleweka na mwanadamu, ambayo ni ya ajabu na yenye hekima—yote si yasiyo ya kawaida? Hata hivyo, unapaswa kujua

kuwa, haijalishi jinsi kisicho cha kawaida, mambo yote yanatekelezwa katika ubinadamu Wake wa kawaida. Mwili wa Mungu umejaa ubinadamu, la sivyo, haungekuwa Mwili wa Mungu katika mwili. Katika wakati huo, Yesu alitenda miujiza mingi sana. Kile ambacho Waisraeli wa wakati huo waliona kilijaa mambo yasiyo ya kawaida; walitazama malaika na wajumbe, na walisikia sauti ya Yehova. Je, haya yote hayakuwa yasiyo ya kawaida? Bila shaka, leo kunao baadhi ya pepo wabaya wanaomdanganya mwanadamu kutumia mambo yasiyo ya kawaida; hilo si chochote bali ni uigaji kwa upande wao, kumpotosha mwanadamu kupitia kwa kazi ambayo kwa sasa haifanywi na Roho Mtakatifu. Watu wengi hufanya miujiza na kuwaponya wagonjwa na kufukuza mapepo; hizi ni kazi za pepo wabaya tu, kwani Roho Mtakatifu hafanyi tena kazi kama hiyo leo na wale wote ambao wameiga kazi ya Roho Mtakatifu kutoka wakati huo kuendelea—wao ni pepo wabaya kweli. Kazi yote iliyotekelezwa Israeli wakati huo ilikuwa ile ya miujiza, ingawa Roho Mtakatifu sasa hafanyi kazi kwa njia hiyo, na kazi yoyotekama hiyo sasa ni kuiga na kujificha kwa Shetani na usumbufu wake. Lakini huwezi kusema kwamba mambo yote ya rohoni ni shughuli ya pepo waovu. Hili linategemea enzi ya kazi ya Mungu. Ni kazi gani inayofanywa na Mungu aliyepata mwili siku hii si ya rohoni? Maneno Yake ni yasiyoeleweka na yasiyofikika kwako, na kazi Yake haiwezi kufanywa na mwanadamu. Kile kilicho katika ufahamu Wake hakiwezi kueleweka na mwanadamu, na wala mwanadamu hawezi kujua maarifa Yake yanatoka wapi. Wengine husema, mimi pia ni wa kawaida kama Wewe, ni kwa nini mimi sijui unachojua Wewe? Mimi ni mzee zaidi na mwingi zaidi wa uzoefu, ilhali Wewe unawezaje kujua kile nisichojua mimi? Haya yote ni yasiyofikika kwa mwanadamu. Kisha kuna wale ambao husema, “Hakuna anayejua kazi iliyotekelezwa Israeli, na hata wafasiri wa Biblia hawawezi kutoa ufafanuzi; mbona Wewe unajua? Haya yote siyo mambo ya miujiza? Hajawahi kupitia maajabu yoyote, ilhali Anayajua yote; Anazungumza na kuonyesha ukweli kwa urahisi sana. Je, hili sio jambo la kimuijiza? Kazi Yake inazidi ile inayofikika kwa mwili. Kazi hiyo haiwezi hasa kutimizwa kwa fikira zozote za mwili na ni isiyowazika kabisa kwa mawazo na fikira ya mwanadamu. Ingawa hajasoma Biblia asilani, Yeye huelewa kazi ya Mungu katika Israeli. Na ingawa Yeye husimama duniani Anapozungumza, Yeye huzungumza kuhusu mafumbo ya mbingu ya tatu. Mwanadamu atazamapo maneno haya, hisia humlelea mwanadamu, “Je, hii siyo lugha ya mbingu ya tatu?” Haya yote siyo mambo yanayozidi kile ambacho mwanadamu wa kawaida anaweza kukifikia? Wakati huo, Yesu alipofanya mfungo wa siku arobaini, hilo halikuwa la rohoni? Ukisema kwamba mfungo wa siku arobaini ni la rohoni na kitendo cha pepo waovu, basi hujamshutumu Yesu? Kabla ya Yesu kutekeleza huduma Yake, Alikuwa kama wanadamu wote wa kawaida. Yeye pia alisoma shuleni; ni vipi vinginevyo ambavyo angejifunza kusoma na kuandika? Mungu alipopata mwili, Roho alijificha ndani ya mwili. Hata hivyo, kama wanadamu wote wa kawaida, ilikuwa lazima Yeye apitie mchakato wa ukuaji, na ni baada tu ya akili na fikira Zake kukomaa na Yeye kuweza kutambua mambo, ndipo

Alifikiriwa kuwa mwanadamu wa kawaida. Ni baada tu ya ubinadamu Wake kukomaa ndipo Angeweza kutekeleza huduma Yake. Angewezaje kutekeleza huduma Yake ilhali ubinadamu Wake ulikuwa bado haujakomaa na fikira Zake zikiwa pungufu? Kwa hakika Hangetarajiwa kutekeleza huduma Yake akiwa na umri wa miaka sita au saba! Mbona Mungu hakujidhihirisha Mwenyewe wazi wakati ambapo Mungu alipata mwili kwanza? Kwa sababu ubinadamu wa mwili Wake ulikuwa bado haujakomaa; mawazo na akili, pamoja na ubinadamu wa kawaida wa mwili huo, havikuwa vimemilikiwa kwa ukamilifu. Kwa sababu hii, ilikuwa lazima bila shaka kwa Yeye kumilikiwa na ubinadamu wa kawaida na maarifa ya kawaida ya mwanadamu wa kawaida mpaka viweze kutosha kufanya kazi Yake katika mwili. Ni wakati huo tu ndipo Angeanza kazi Yake, la sivyo ingekuwa lazima Yeye aendeleo kukua. Kama Yesu angeanza kazi Yake akiwa na umri wa miaka saba au minane, mwanadamu hangemchukulia Yeye kuwa kioja? Wanadamu wote hawangemfikiria Yeye kuwa mtoto tu? Ni nani angemwona Yeye kuwa wa kuridhisha? Mtoto wa umri wa miaka saba au minane hakuwa mrefu kuliko mimbari aliyosimamia nyuma yake—alifaa kuhubiri? Kabla ya ubinadamu Wake wa kawaida kukomaa, Hangeweza kufanya kazi. Kuhusu ubinadamu Wake ambao bado haukuwa umekomaa, sehemu kubwa ya kazi Yake haikuweza kutimizwa kabisa. Kazi ya Roho wa Mungu katika mwili pia inaongozwa na kanuni zake. Ni wakati tu Anapojitayarisha na ubinadamu wa kawaida ndipo Anapoweza kufanya kazi na kumwongoza Baba. Hapo tu ndipo Angeanza kazi Yake. Utotoni Mwake, Yesu hangeelewa mengi ya yale yaliyotendeka katika wakati wa kale, na ni kwa kuuliza waalimu ndani ya sinagogi tu ndipo Alipata kuelewa. Iwapo Angeanza kazi Yake pindi Alipojua kuzungumza, Angewezaje kutofanya makosa yoyote? Mungu Angewezaje kufanya makosa? Kwa hivyo, ilikuwa tu baada ya kuweza ndipo Alianza kazi Yake; Hakufanya kazi yoyote hadi Alipokuwa na uwezo wa kuyatekeleza. Akiwa na miaka 29, Yesu Alikuwa Amekomaa vya kutosha na ubinadamu Wake kutosha kutekeleza kazi Aliyopaswa kutekeleza. Ilikuwa hapo tu ndipo Roho wa Mungu Akaanza kirasmi kufanya kazi ndani Yake. Katika wakati huo, Yohana alikuwa ametenda kazi kwa miaka saba kwa kutayarisha njia Yake, na baada ya kumaliza kazi Yake, Yohana alitupwa gerezani. Mzigo wote basi ukamwangukia Yesu. Kama Angetekeleza kazi hii Akiwa na miaka 21 ama 22, Alipokuwa bado hana ubinadamu wa kutosha na Ameingia tu utu uzima, Akiwa bado haelewi mambo mengi, hangeweza kuchukua udhibiti. Katika wakati huo, Yohana alikuwa ameshafanya kazi yake kwa muda kabla Yesu kuanza kazi Yake katika miaka Yake ya katikati. Katika miaka hiyo, ubinadamu Wake wa kawaida ulikuwa unatosha kufanya kazi Aliyopaswa kufanya. Sasa, Mungu aliyepata mwili pia ana ubinadamu wa kawaida naingawa sio uliokomaa ukilinganishwa na wale walio wazee miongoni mwenu, ubinadamu huu tayari unatosha jinsi ulivyo kufanya kazi Yake; hali ya kazi Anayofanya leo siyo sawa kabisa na ile ya Yesu. Kwa nini Yesu aliwachagua mitume kumi na wawili? Yote ilikuwa ni kwa usaidizi wa kazi Yake na pamoja na hiyo. Kwa upande mmoja, ilikuwa ni kuweka msingi wa kazi Yake

wakati huo, na vilevile pia kufanya hivyo kwa ajili ya kazi Yake iliyofuata. Kwa mujibu wa kazi wakati huo, uchaguzi wa wanafunzi kumi na wawili ulikuwa kusudi la Yesu, na vilevile la Mungu Mwenyewe. Aliamini wanafunzi kumi na wawili walipaswa kuchaguliwa kisha waongozwe kuhubiri mahali kote. Lakini hakuna haja ya hili miongoni mwenu siku hii! Kazi ya Mungu mwenye mwili katika mwili na kanuni nyingi. Kuna mengi ambayo mwanadamu haelewi, ilhali mwanadamu anatumia mara kwa mara fikira zake kuipima au kuwa na matarajio mengi kutoka Kwake. Hata wakati huu kunao wengi wasiofahamu kabisa kuwa maarifa yao ni ya fikira zao tu. Haijalishi enzi ama mahali ambapo Mungu anapata mwili, kanuni za kazi Yake katika mwili Wake hazibadiliki. Hawezi kuwa Mwili kisha Avuke mwili kwa kufanya kazi; zaidi, hawezi kuwa mwili kisha Akose kufanya kazi katika mwili wa kawaida wa binadamu. Vinginevyo, umuhimu wa Mungu kupata mwili utapotea na kuwa bure, na Neno kuwa mwili itakuwa haina maana. Zaidi ya hayo, Baba tu Aliye mbinguni (Roho) Anajua kuhusu Mungu katika mwili wa Mungu, na sio mwingine, sio hata mwili Mwenyewe ama wajumbe wa mbinguni. Hivyo, kazi ya Mungu katika mwili ni ya kawaida zaidi na bora kueleza Neno kuwa mwili; mwili unamaanisha mwanadamu wa kawaida.

Wengine wanaweza kushangaa, mbona enzi ikaribishwe na Mungu Mwenyewe? Kiumbe kilichoumbwa hakiwezi kusimama kwa niaba Yake? Nyote mnafahamu kuwa Mungu Anakuwa mwili hasa kwa ajili ya kuikaribisha enzi mpya, na, kwa hakika, Anapoikaribisha enzi mpya, Atakuwa Ameikamilisha enzi ya kale wakati uo huo. Mungu ndiye Mwanzo na tena Mwisho; ni Yeye Mwenyewe ndiye Anayeanzisha kazi Yake na hivyo lazima iwe ni Yeye Mwenyewe Anayemaliza enzi ya kale. Huo ndio ushahidi kuwa Yeye humshinda Shetani na huishinda dunia. Kila wakati Yeye Mwenyewe Anapofanya kazi miongoni mwa mwanadamu, ni mwanzo wa mapigano mapya. Bila mwanzo wa kazi mpya, kwa kawaida hakutakuwa na kikomo kwa enzi ya kale. Na bila kikomo kwa enzi ya kale ina maana kuwa vita na Shetani havijafika mwisho. Ni kama tu Mungu Mwenyewe Anakuja miongoni mwa mwanadamu na kutenda kazi mpya ndipo mwanadamu atakapoweza kujitoa kutoka katika umiliki wa Shetani na kupata maisha na mwanzo mpya. Vinginevyo, mwanadamu ataishi milele katika wakati wa kale na milele kuishi katika ushawishi wa kale wa Shetani. Katika kila enzi inayoongozwa na Mungu, sehemu ya mwanadamu huwekwa huru, na hivyo, mwanadamu huendelea na kazi ya Mungu kuelekea enzi mpya. Ushindi wa Mungu ni ushindi kwa wale ambao humfuata Yeye. Kama binadamu wa kuumbwa angepewa usukani wa kutimiza enzi, basi iwe kutoka kwa mtazamo wa mwanadamu ama Shetani, hii ni kama kupinga au kusaliti Mungu, na hivyo kazi ya mwanadamu ingegeuka kuwa chombo kwa Shetani. Mwanadamu anapotii na kumfuata Mungu katika enzi iliyokaribishwa na Mungu Mwenyewe tu ndipo Shetani angeshawishiwa kabisa, kwani hiyo ndiyo kazi ya kiumbe aliyeumbwa. Kwa hivyo Nasema kuwa mnafaa tu kufuata na kutii, na

hakuna kingine kitakachoulizwa kutoka kwenu. Hiyo ndiyo maana ya kusema kila mmoja kuendeleza kazi na kufanya kazi Yake. Mungu hufanya kazi Yake Mwenyewe na Yeye hahitaji mwanadamu kufanya kazi Yake kwa niaba Yake, na wala hajishughulishi katika kazi ya viumbe. Mwanadamu anafanya kazi yake na haingilii kati kazi ya Mungu, na huo ndio utii wa kweli na ushahidi kuwa Shetani ameshindwa. Baada ya Mungu Mwenyewe kukaribisha enzi mpya, Yeye Mwenyewe hafanyi kazi tena kati ya mwanadamu. Ni wakati huo tu ndipo mwanadamu anaingia rasmi katika enzi mpya kufanya kazi yake na kutekeleza misheni yake kama kiumbe aliyeumbwa. Hivyo ndivyo zilivyo kanuni za kazi zisizowezwa kukiukwa na yeyote. Kufanya kazi katika njia hii pekee ndio yenye busara. Kazi ya Mungu hufanywa na Mungu Mwenyewe. Ni Yeye ndiye Anayeweka kazi katika mwendo, na pia Yeye ndiye Anayemaliza. Ni Yeye ndiye hupanga kazi, na pia Yeye ndiye Anayesimamia, na zaidi ya hayo, ni Yeye ndiye Anayeleta kazi kuzaa matunda. Ni ilivyoandikwa katika Biblia, “Mimi ndiye Mwanzo na Mwisho: Mimi ndiye Mpanzi na Mvunaji.” Yote yanayohusiana na usimamizi wa kazi Yake yanafanywa na mkono Wake. Yeye ndiye Mtawala wa mpango wa miaka elfu sita; hakuna anayeweza kufanya kazi Yake kwa niaba Yake ama kuleta kazi Yake hadi mwisho, kwani Yeye ndiye Aliye katika uongozi wa yote. Kwa kuwa Aliumba dunia, Ataongoza ulimwengu mzima kuishi katika nuru Yake, na Atamaliza enzi yote na kuleta mpango Wake wote kwa mafanikio!

Fumbo la Kupata Mwili (2)

Katika wakati ambapo Yesu Alifanya kazi Uyahudi, Aliifanya wazi, lakini sasa, Nazungumza na Kufanya kazi kati yenu kwa siri. Wasioamini hawana ufahamu wowote. Kazi Yangu kati yenu imetengwa kutoka kwa nyingine. Maneno haya, kuadibu huku na hukumu hii, vinajulikana tu kwako na sio mwingine. Kazi hii yote inatendeka kati yenu na kuonekana tu kwenu; hakuna yeyote asiyeamini anayefahamu haya, kwani muda haujafika. Wanadamu hao wako karibu kufanywa wakamilifu baada ya kuvumilia adibu, lakini wale walio nje hawajui lolote juu yake. Kazi hii imefichwa sana! Kwao, Mungu mwenye mwili ni siri, lakini kwa wale walio katika mkondo, Anaweza kuchukuliwa kuwa wazi. Ingawa kwa Mungu yote ni wazi, yote yanakuwa wazi na yote yanaachiliwa, haya tu ni ya ukweli kwa wale wanaomwamini, na hakuna kitu kinachofanywa kujulikana kwa wale wasioamini. Kazi inayofanywa kwa sasa miongoni mwenu na huko Uchina imefungwa vikali, ili kuwazuia wasijue. Wakipata kujua, kinachowangojea ni shutuma na mateso. Hawataamini. Kufanya kazi katika taifa la joka kuu jekundu, mahali palipo nyuma zaidi, sio kazi rahisi. Kama kazi hii ingewekwa wazi na kujulikana, basi ingekuwa vigumu kuendelea. Hatua hii ya kazi haiwezi kuendelea katika sehemu hii. Wangestahimili vipi kama kazi hii ingeendelezwa kwa uwazi? Hii haingeleta hata hatari kubwa zaidi? Kama kazi hii haingefichwa, na badala Yake kuendelea kama wakati wa Yesu Alivyowaponya wagonjwa na kufukuza mapepo kwa njia ya kustaajabisha, basi si

ingekuwa tayari “imeshanyakuliwa” na ibilisi? Je, wangestahimili uwepo wa Mungu? Kama sasa ningeingia kwenye sinagogi kuwahadhiria wanadamu, je, si ninge kuwa nimeshapasuliwa katika vipande kitambo? Na ikiwa hivyo, kazi Yangu itawezaje kuendelea kufanyika? Sababu ambayo ishara na miujiza haitendeki wazi wazi ni kwa ajili ya kujificha. Kwa hivyo kazi Yangu haiwezi kuonekana, kujulikana wala kugunduliwa na wasioamini. Iwapo hatua hii ya Kazi ingefanyika kwa njia sawa na kazi ya Yesu katika Enzi ya Neema, haingekuwa thabiti sana. Kwa hivyo, kazi hii kufichwa namna hii ni ya manufaa kwenu na kwa kazi yote. Wakati kazi ya Mungu duniani inafika kikomo, kumaanisha, wakati kazi hii katika siri inakamilika, hatua hii ya kazi italipuka na kuwa wazi. Watu wote watajua kwamba kuna kundi la washindi ndani ya taifa la Uchina; kila mwanadamu atafahamu kuwa Mungu katika mwili yuko Uchina na kwamba kazi Yake imefika kikomo. Hapo tu ndipo kutampambazukia mwanadamu: Ni kwa nini taifa la Uchina halijaonyesha kudhoofika wala kuporomoka? Inaonekana kuwa Mungu anaendeleza kazi Yake binafsi katika taifa la China na amefanya kuwa kamilifu kundi la watu na kuwafanya washindi.

Mungu mwenye mwili Anajidhihirisha mwenyewe kwa watu kadhaa wanaomfuata Anapofanya kazi Yeye binafsi, na sio kwa viumbe wote. Alijifanya mwili ili Akamilishe hatua ya kazi Yake, na sio ili amwonyeshe mwanadamu mfano Wake. Hata hivyo, kazi Yake lazima ifanywe na Yeye binafsi, kwa hivyo inalazimu Afanye kazi hiyo katika mwili. Kazi hii inapokamilika, Ataondoka duniani; Hawezi kusalia duniani kwa muda mrefu kwa hofu ya kuzuia kazi inayokuja. Anachokionyesha kwa halaiki ni tabia Yake ya haki na matendo Yake yote, na sio umbo la wakati Amejifanya mwili mara mbili, kwa maana mfano wa Mungu unaweza tu kuonyeshwa kupitia kwa tabia Yake, na si kubadilishwa na mfano wa mwili Wake wa nyama. Mfano wa mwili Wake wa nyama huonyeshwa kwa watu wachache tu, kwa wale wanaomfuata Anapofanya kazi katika mwili. Hiyo ndio maana kazi inayofanywa wakati huu inafanywa kwa siri. Ni kama tu vile Yesu alivyojionyesha kwa Wayahudi pekee yao Alipofanya kazi Yake, na hakujionyesha hadharani kwa mataifa mengine. Hivyo, pindi Alipomaliza kazi Yake, Aliondoka miongoni mwa wanadamu na hakukawia; kwa wakati uliofuata Hakujionyesha kwa nafsi Yake kwa mwanadamu, bali kazi iliendeshwa moja kwa moja na Roho Mtakatifu. Mara tu kazi ya Mungu katika mwili inapokamilika, Anaondoka katika dunia ya mwanadamu, na kamwe Hafanyi tena kazi sawa na ile Aliyofanya Akiwa katika mwili. Kazi inayofuata hufanywa na Roho Mtakatifu moja kwa moja. Wakati huu, mwanadamu hawezi kuona mfano Wa Mungu katika mwili; Yeye Hajionyeshi wazi kwa mwanadamu hata kidogo, na daima Anabaki mafichoni. Muda wa kazi ya Mungu mwenye mwili ni mchache, ambayo lazima ifanywe katika Enzi bayana, muda, taifa na kati ya watu bayana. Kazi kama hiyo inawakilisha tu kazi ya wakati wa Mungu katika mwili, na inalenga enzi fulani, ikiwakilisha kazi ya Roho wa Mungu katika enzi moja hasa, na sio ujumla wa kazi Yake. Kwa hivyo, umbo la Mungu mwenye mwili

halitaonyeshwa kwa kila mwanadamu. Kinachoonyeshwa kwa halaiki ni haki ya Mungu na tabia Yake kwa ukamilifu, na wala sio mfano Wake Alipokuwa mwili mara mbili. Sio sura inayoonyeshwa kwa mwanadamu, wala mifano yote miwili ikijumlishwa. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba mwili wa Mungu uondoke duniani baada ya kukamilisha kazi Anayohitajika kufanya, kwa kuwa Anakuja tu kufanya kazi Anayopaswa kufanya, na sio kuwaonyesha wanadamu mfano wa umbo Lake. Ingawa umuhimu wa kuingia katika mwili umeshatimizwa na Mungu mara mbili Akijifanya mwili na nyama, bado hatajionyesha wazi kwa taifa ambalo halijawahi kumwona mbeleni. Yesu hatajionyesha Mwenyewe kamwe mara nyingine kwa Wayahudi kama Jua la haki, wala Hataupanda Mlima wa Mizeituni na kuonekana kwa watu wote: yote ambayo Wayahudi huona ni taswira Yake wakati wa kipindi Chake katika Uyahudi. Hili ni kwa sababu kazi ya Yesu aliyepata mwili iliisha kitambo sana miaka elfu mbili iliyopita; Hatarudi Uyahudi katika sura ya Myahudi, sembuse kujionyesha katika sura ya Myahudi kwa nchi yoyote ya Mataifa, kwani sura ya Yesu aliyepata mwili ni sura ya Myahudi tu, na siyo sura ya Mwana wa Adamu ambayo Yohana alikuwa ameiona. Ingawa Yesu aliwaahidi wafuasi Wake kwamba Angerudi tena, Hatajionyesha tu Mwenyewe katika sura ya Myahudi kwa wote walio katika nchi za Mataifa. Mnapaswa kujua kwamba kazi ya Mungu katika mwili inafaa kufungua enzi mpya. Kazi hii ni ya muda wa miaka michache tu, na Hawezi kukamilisha kazi yote ya Roho wa Mungu. Hii ni sawia na vile umbo la Yesu kama Myahudi linaweza tu kuwakilisha mfano wa Mungu alivyofanya kazi katika Yudea, na Angefanya tu kazi ya msalabani. Wakati ambao Yesu Alikuwa katika mwili, Hangefanya kazi ya kutamatisha enzi au kumwangamiza mwanadamu. Kwa hivyo, baada ya kusulubiwa na kukamilisha kazi Yake, Alipaa juu na daima Akajificha kutoka kwa mwanadamu. Kutoka wakati huo kuendelea, wale waumini wa mataifa waliweza tu kuiona picha Yake ambayo walibandika kwenye kuta zao, na sio udhihirisho wa Bwana Yesu. Picha hii imechorwa na mwanadamu tu, na si mfano ambao Mungu Mwenyewe Alimwonyesha mwanadamu. Mungu Hatajionyesha kwa halaiki wazi wazi katika mfano ambao Yeye Alikuwa nao mara mbili Akiwa katika mwili. Kazi Anayofanya miongoni mwa wanadamu ni kuwaruhusu kuelewa tabia Yake. Yote haya yanaonyeshwa kwa mwanadamu kwa njia ya kazi za enzi tofauti; yanakamilishwa kupitia tabia ambazo Ameziweka wazi na kazi ambayo Amefanya, na bali si kupitia kwa udhihirisho wa Yesu. Hiyo ni kusema, umbo la Mungu halionyeshwi kwa mwanadamu kupitia katika mfano wa Mungu mwenye mwili, lakini ni kwa kupitia katika kazi iliyotekelezwa na Mungu mwenye mwili wa sura na umbo; na kupitia kazi Yake, mfano Wake unaonekana na tabia Yake inajulikana. Huu ndio umuhimu wa kazi Angependa kufanya katika mwili.

Wakati kazi ya Alipokuwa mwili mara mbili inakamilika, Anaanza kuonyesha tabia Yake ya haki katika mataifa, Akiruhusu halaiki ione mfano wa umbo Lake. Anapenda kudhihirisha

tabia Yake, na kupitia katika hili Aweke wazi tamati za aina tofauti ya wanadamu, hapo kuifikisha mwisho kabisa enzi nzee. Kazi Yake katika mwili haitendeki katika sehemu pana (kama vile Yesu Alivyofanya kazi katika sehemu ya Yuda peke Yake, na leo hii Ninafanya kazi miongoni mwenu pekee) kwa sababu kazi Yake katika mwili ina mipaka na kingo. Anafanya tu kazi ya muda mchache katika mfano wa kawaida na mwili wa kawaida, badala ya kufanya kazi ya milele kupitia kwa Mungu mwenye mwili, ama kufanya kazi ya kuwaonekana watu wote wa mataifa. Kazi hii katika mwili lazima izuiliwe katika mawanda (kama vile kufanya kazi katika Yuda ama kati Yenu), kisha kupanua kazi iliyofanyika katika mipaka hii. Bila shaka, kazi ya upanuzi huu huendeshwa na Roho Mtakatifu moja kwa moja na haiwezi kuwa kazi ya mwili Wake wa nyama. Kwa maana kazi katika mwili iko na mipaka na haiwezi kuenea katika pembe zote za ulimwengu. Hauwezi kuyatekeleza haya. Kupitia kwa kazi katika mwili, Roho Wake hutekeleza kazi inayofuatia. Kwa hivyo, kazi inayofanywa katika mwili ni ya matayarisho inayotekelezwa ndani ya mipaka; Roho Wake kisha Anaendeleza kazi hii, na kuipanua.

Mungu huja tu katika dunia hii kufanya kazi ya kuongoza enzi; kufungua enzi mpya na kutamatisha enzi ya zamani. Hajakuja kuishi kulingana na maisha ya mwanadamu wa kawaida kwa kikamilifu, kupitia Mwenyewe raha na machungu ya maisha kama mwanadamu, au kumfanya mtu fulani mkamilifu kwa mkono Wake au kumtazama binafsi mtu Fulani anavyokua. Hii sio kazi Yake; kazi Yake ni kufunua tu enzi mpya na kutamatisha enzi iliyotangulia. Hiyo ina maana, Atafungua enzi mpya, akamilishe iliyotangulia, amshinde shetani kwa kufanya kazi Yake binafsi. Kila mara Anapotekeleza kazi Yeye Mwenyewe, ni kana kwamba Anakanyaga mguu wake katika uwanja wa vita Katika mwili, kwanza Anaishinda dunia kisha Anatawala juu ya Shetani; Anachukua utukufu wote na kufungua pazia kwa kazi ya enzi yote elfu mbili, na kuwapa binadamu wote duniani njia ya kweli ya kufuata, na maisha ya amani na furaha. Hata hivyo, Mungu hawezi kuishi na mwanadamu duniani kwa muda mrefu, kwa maana Mungu ni Mungu, ni si kama mwanadamu kamwe. Hawezi kuishi urefu wa maisha ya mwanadamu wa kawaida, hiyo ina maana, Hawezi kuishi duniani kama mwanadamu ambaye si wa kawaida, kwa maana Yuko na sehemu ndogo ya ubinadamu wa kawaida wa mtu wa kawaida kumuwezesha kuishi vile. Kwa maneno mengine, Mungu anawezaje kuanzisha familia, kuwa na kazi na kulea watoto duniani? Je, si hii itakuwa ni aibu? Kwamba Yeye amejaliwa na ubinadamu wa kawaida ni kwa minajili tu ya kutekeleza kazi Yake kwa njia ya kawaida, na sio kumuwezesha Yeye kuwa na familia na kazi kama mtu wa kawaida. Hisia Zake za kawaida, mawazo ya kawaida, na kula kwa kawaida na nguo za mwili Wake yanatosha kuthibitisha kuwa Yuko na ubinadamu wa kawaida; hakuna haja Yake kuwa na familia au kazi ili athibitishe kwamba Yeye kweli yuko na ubinadamu wa kawaida. Hiyo haina maana hata kidogo! Mungu anakuja duniani, kumaanisha Neno linageuka kuwa mwili; Kwa urahisi Anamruhusu mwanadamu kulielewa neno Lake na

kuliona neno Lake, hiyo ni, kumruhusu mwanadamu kuona kazi inayotekelezwa na mwili. Nia Yake sio kwamba wanadamu wauchukue mwili Wake kwa njia Fulani, bali kwamba mwanadamu awe mtiifu mpaka mwisho, kumaanisha, aweze kutii maneno yote yanayotoka katika kinywa Chake, na kunyenyekea na kukubali kazi yote Anayofanya. Yeye Anafanya kazi katika mwili tu; Yeye hamuulizi mwanadamu kwa kujua aabudu ukuu na utakatifu wa mwili Wake, bali anamwonyesha mwanadamu hekima ya kazi Yake na mamlaka yote Aliyo nayo. Kwa hivyo, ingawa Anao ubinadamu wa kipekee, Hafanyi matangazo yoyote, na Anatilia tu maanani kazi ambayo Anapaswa kufanya. Mnapaswa kujua ni kwa nini Mungu Alipata mwili na ilhali hatangazi wala kushuhudia juu ya ubinadamu Wake wa kawaida, lakini badala yake Anatekeleza tu kazi ambayo Angependa kufanya. Hii ndio sababu mnaona tu uwepo wa uungu katika Mungu mwenye mwili, kwa sababu Hatangazi kuwa Kwake katika mwili ndio mwanadamu aige. Wakati tu mwanadamu anamwongoza mwanadamu ndipo anapozungumzia kuhusu kile alichokama binadamu, ndivyo apate heshima na utii wao vyema zaidi na hivyo kufanikisha uongozi wa wengine. Kinyume na hilo, Mungu huwashinda watu kupitia katika kazi Yake pekee (hiyo ni, kazi isiyoweza kufanywa na mwanadamu); hakuna shaka ya mwanadamu kuvutiwa na Yeye au kumfanya mwanadamu amwabudu. Yote Anayofanya ni kuweka tu katika mwanadamu hisia za uchaji Kwake au kumfanya mwanadamu aweze kujua kuhusu kutowezekana kwa kumchunguza Yeye. Hakuna haja ya Mungu kumpendeza mwanadamu. Kile anachohitaji ni kuwa wewe umheshimu na kumwabudu mara tu unaposhuhudia tabia Yake. Kazi ambayo Mungu hufanya ni Yake mwenyewe; haiwezi kufanywa na mwanadamu badala Yake, wala kuweza kutimizwa na mwanadamu. Ni Mungu Mwenyewe tu ndiye Anaweza kufanya kazi Yake mwenyewe na kuanzisha enzi mpya ili kumwongoza mwanadamu katika maisha mapya. Kazi ambayo Yeye hufanya ni kumwezesha mwanadamu kupokea maisha mapya na kuingia katika enzi mpya. Kazi nyingine yote hupokezwa kwa wale wanadamu wa ubinadamu wa kawaida na ambao wanapendwa na wengine. Kwa hivyo, katika Enzi ya Neema, Alimaliza kazi ya miaka elfu mbili katika miaka mitatu na nusu pekee wakati wa miaka Yake thelathini na mitatu ndani ya mwili. Wakati ambapo Mungu atakuja duniani kutekeleza kazi Yake, Yeye kila mara hukamilisha kazi ya miaka elfu mbili au ya enzi nzima katika muda mfupi sana wa miaka michache. Yeye hachelewi, na Hasimami; Yeye hufupisha tu kazi ya miaka mingi ili ikamilishwe katika miaka michache tu mifupi. Hili ni kwa sababu kazi ambayo Yeye hufanya Mwenyewe ni kuifungua tu njia mpya na kuiongoza enzi mpya.

Fumbo la Kupata Mwili (3)

Wakati ambapo Mungu huitekeleza kazi Yake, Yeye haji kujishughulisha katika ujenzi wowote au mabadiliko; Yeye huja kutimiza huduma Yake. Kila wakati Anapopata mwili, ni kwa ajili tu ya kufanikisha hatua ya kazi na kuifungua enzi mpya. Sasa Enzi ya Ufalme imefika, na

mafundisho ya ufalme. Hatua hii ya kazi si kazi ya mwanadamu, si ya kumfanyia kazi mwanadamu kwa kiwango fulani; ni kuimaliza sehemu ya kazi ya Mungu tu. Kazi Yake si kazi ya mwanadamu, si kufikia matokeo fulani katika kumfanyia kazi mwanadamu kabla ya kuondoka duniani; ni kutimiza huduma Yake kwa ukamilifu na kuimaliza kazi ambayo Anapaswa kuifanya, ambayo ni kutengeneza mipango ya kufaa ya kazi Yake duniani, na hivyo kupata kutukuka. Kazi ya Mungu mwenye mwili ni tofauti na ile ya wale wanaotumiwa na Roho Mtakatifu. Mungu anapofanya kazi Yake duniani, Yeye anajali kutimilika kwa huduma Yake pekee Yake. Na kwa mambo mengine yasiyohusiana na huduma Yake, Yeye kimatendo hajishughulishi hata kidogo, hata kwa kiwango cha kuzipa mgongo shughuli hizo. Yeye hufanya tu kazi Anayopaswa kufanya, na hajishughulishi na kazi ambayo mwanadamu anapaswa kufanya. Kazi Anayofanya ni ile tu inahusiana na enzi Aliyomo na huduma Anayopaswa kukamilisha, kana kwamba mambo mengine yote si jukumu Lake. Yeye hajijazi na maarifa ya kawaida kuhusu jinsi ya kuishi kama mwanadamu, na Hajifunzi mahusiano ya jamii au mambo yoyote ambayo mwanadamu anaelewa. Hajishughulishi kamwe na mambo ambayo mwanadamu anapaswa kujua na Anafanya tu kitu ambacho ni jukumu Lake. Kwa hivyo, mwanadamu anavyoona, Mungu mwenye mwili ni mwenye upungufu katika mambo mengi mno, hata kwa kiasi kwamba Anavipa mgongo vingi ambavyo mwanadamu anapaswa kuwa navyo, na kwamba hana ufahamu wa mambo kama hayo. Mambo kama ufahamu wa maisha ya kawaida, na vile vile kanuni za tabia na kuhusiana na wengine, huonekana kuwa hazina uhusiano Kwake. Hata hivyo, huwezi kuona kutoka kwa Mungu mwenye mwili tabia zozote zisizo za kawaida. Hiyo ni kusema, ubinadamu Wake unadumisha maisha Yake kama mwanadamu wa kawaida na fikira za kawaida za ubongo Wake, na kumpa uwezo wa kutofautisha kati ya mazuri na mabaya. Hata hivyo, Hajajazwa na kingine chochote, yote ambayo ni ya wanadamu (walioumbwa) pekee. Mungu anapata mwili ili kukamilisha huduma Yake pekee. Kazi Yake inaelekezwa kwa enzi nzima na sio kwa mtu binafsi au mahali fulani. Kazi Yake inaelekezwa kwa ulimwengu mzima. Huu ndio mwelekeo wa kazi Yake na kanuni Anayofuata katika kazi Yake. Hii haiwezi kubadilishwa na yeyote, na mwanadamu hawezi kuhusika kwa sehemu yoyote. Kila wakati ambapo Mungu hupata mwili, Yeye huja pamoja na kazi ya enzi hiyo, na sio dhamira ya kuishi ubavuni mwa mwanadamu kwa miaka ishirini, thelathini, arobaini, au hata miaka sabini, themanini ili waweze kuelewa bora zaidi na kupata utambuzi Kwake. Hakuna haja ya hilo! Kufanya hivyo hakungeweza katu kuzidisha ufahamu ambao mwanadamu anao wa tabia ya asili ya Mungu; badala yake, kungeongeza tu kwa fikira zao na kufanya fikira na mawazo ya mwanadamu yawe kuukuu. Na kwa hiyo nyote mnapaswa kuelewa hasa ni nini kazi ya Mungu aliyepata mwili. Yawezekana kwamba hamyaelewi maneno Yangu: “Siji kuyapitia maisha ya mwanadamu wa kawaida”? Je, mmesahau maneno: “Mungu haji duniani kuishi maisha ya mwanadamu wa kawaida”? Hamlielewi kusudi la Mungu kupata mwili, wala hamjui maana ya

“Mungu angekujaje duniani na dhamira ya kuyapitia maisha ya kiumbe aliyeumbwa?” Mungu anakuja tu duniani kukamilisha kazi Yake, na kwa hivyo Kazi Yake duniani ni ya muda mfupi. Haji duniani na nia ya Roho wa Mungu kukuza mwili Wake kuwa mkuu wa kipekee wa kanisa. Mungu anapokuja duniani, ni Neno ambalo kugeuka kuwa mwili; mwanadamu, hata hivyo, hajui kuhusu kazi Yake na kwa nguvu anaona Yeye kuwa sababu ya mambo. Lakini nyote mnapaswa kufahamu kuwa Mungu ni Neno lililogeuka kuwa mwili, na sio mwili uliokuzwa na Roho wa Mungu ili kusimamia nafasi ya Mungu kwa ufupi. Mungu Mwenyewe hakuzwi, ila ni Neno kugeuka mwili, na leo hii Anatekeleza kazi Yake kirasmi miongoni mwenu. Nyote mwajua na kukubali kwamba kupata mwili kwa Mungu ni ukweli, lakini mnajidai kuwa na ufahamu ambao kwa kweli hamna. Ninyi hamthamini kabisa kazi ya Mungu aliyepata mwili au umuhimu na kiini cha Yeye kupata mwili, na husimulia kwa urahisi tu maneno ambayo hunenwa na wengine. Je, unaamini kwamba Mungu aliyepata mwili ni kama unavyodhani.

Mungu hugeuka mwili ili tu Aiongoze enzi na Aanzishe kazi mpya. Lazima muelewe hoja hii. Hii ni tofauti kabisa na kazi ya mwanadamu, na mawili haya hayawezi kuzungumzwa kwa pamoja. Mwanadamu anahitaji muda mrefu wa kukuzwa na kufanywa mkamilifu kabla mwanadamu aweze kutumiwa kutekeleza kazi, na ubinadamu wa hali ya juu unahitajika. Mwanadamu hapaswi kudumisha hali yake ya ubinadamu wa kawaida tu, bali pia mwanadamu zaidi ya hapo lazima aelewe kanuni nyingi na sheria za tabia kabla ya mengine, na zaidi ya hayo lazima ajifunze zaidi kuhusu hekima na maadili ya mwanadamu. Haya ndiyo mwanadamu lazima kujengwa nayo. Hata hivyo, hivi sivyo ilivyo na Mungu mwenye mwili, kwa maana kazi Yake haimwakilishi mwanadamu na wala si ya binadamu; bali ni dhihirisho la moja kwa moja la hali Yake na utekelezaji wa moja kwa moja wa kazi Anayopaswa kufanya. (Kwa kawaida, kazi Yake hufanyika wakati inapaswa kufanyika, na sio tu wakati wowote kiholela. Badala Yake, kazi Yake hufanyika wakati ambapo ni wakati wa kukamilisha huduma Yake). Yeye hajihusishi katika maisha ya mwanadamu wala katika kazi ya mwanadamu, hiyo inamaanisha, ubinadamu Wake haujengwi na yoyote kati ya haya (lakini hili haliathiri kazi Yake). Anatimiza huduma Yake tu ikiwa wakati umewadia wa kufanya hivyo; haijalishi hali Aliyomo, Yeye huendelea mbele na kazi Anayopaswa kufanya. Haijalishi mwanadamu anajua nini kumhusu, au maoni ya mwanadamu kumhusu, kazi Yake haiathiriki. Hii ni kama tu vile Yesu Alivyofanya kazi Yake; hakuna aliyejua Yeye ni nani, lakini Aliendelea tu mbele na kazi Yake. Mambo haya hayakumuathiri katika utendaji wa kazi Yake Aliyopaswa kufanya. Kwa hivyo, Hakukiri au kutangaza kuwa Yeye ni nani, na Yeye alimfanya mwanadamu Amfuate tu. Kwa kawaida, huu haukuwa tu uvumilivu wa Mungu; ilikuwa ni njia ambayo Yesu anafanya kazi katika mwili. Angeweza tu kufanya kazi kwa namna hii, kwani mwanadamu hangeweza kumtambua Yesu kwa jicho la kawaida. Na hata kama mwanadamu angeweza, mwanadamu hangeweza kusaidia katika

kazi Yake. Zaidi ya hayo, hakugeuka mwili ili mwanadamu apate kujua mwili huu Wake; ilikuwa ni kwa ajili ya kufanya kazi Yake na kukamilisha huduma Yake. Kwa sababu hii, hakutilia maanani hali ya kufanya Ajulikane. Alipokamilisha kazi Aliyopaswa kufanya, utambulisho Wake na hadhi Yake vilijulikana wazi kwa mwanadamu. Mungu mwenye mwili hukaa kimya na hafanyi matangazo yoyote. Yeye hajishughulishi na mwanadamu au vile mwanadamu anaendelea katika kumfuata, na yeye husonga tu mbele katika kutimiza huduma Yake na kufanya kazi Anayopaswa kufanya. Hakuna Anayeweza kusimama mbele ya njia ya kazi Yake. Wakati muda unawadia wa kazi Yake kukamilika, ni muhimu kazi hiyo ikamilike na kufikishwa kikomo. Hakuna anayeweza kusema vinginevyo. Baada tu ya Yeye kuondoka kutoka kwa mwanadamu baada ya kukamilisha kazi Yake ndipo mwanadamu ataelewa kazi Anayofanya, ingawa hataifahamu kikamilifu. Na itachukua muda mrefu ndipo mwanadamu aelewe nia Yake Alipofanya kazi hiyo mara ya kwanza. Kwa maneno mengine, kazi ya enzi ambapo Mungu anageuka mwili imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu moja ni kupitia katika kazi na maneno ya Mungu mwenye mwili Mwenyewe. Pindi tu huduma ya mwili Wake imetimika kikamilifu, sehemu nyingine ya kazi inatakiwa kutekelezwa na Roho Mtakatifu; basi utakuwa wakati wa mwanadamu kutimiza wajibu wake, kwa maana Mungu ameshafungua njia tayari, na lazima itembelewe na mwanadamu mwenyewe. Hiyo ni kusema, Mungu anageuka kuwa mwili ili kutekeleza sehemu moja ya kazi Yake, na inaendelezwa kwa urithi na Roho Mtakatifu na vile vile wale watu wanaotumiwa na Roho Mtakatifu. Kwa hivyo mwanadamu anapaswa kujua kazi ya msingi inayopaswa kutekelezwa na Mungu mwenye mwili katika hatua hii ya kazi. Mwanadamu lazima aelewe hasa umuhimu wa Mungu kugeuka kuwa mwili na kazi Anayopaswa kufanya, badala ya kumuuliza Mungu ni nini kinachotakiwa kwa mwanadamu. Haya ni makosa ya mwanadamu, na vile vile fikira, na zaidi ya hayo, ni kutotii kwake.

Mungu anakuwa mwili bila nia ya kumfanya mwanadamu apate kuujua mwili Wake, ama kukubali mwanadamu kutofautisha tofauti kati ya mwili wa Mungu mwenye mwili na ule wa mwanadamu; Mungu hapati mwili ili kufunza mwanadamu uwezo wa utambuzi, na zaidi nia ya mwanadamu kumwabudu Mungu mwenye mwili, ambayo kupitia kwayo atapata utukufu mkuu. Hakuna kati ya haya yaliyo mapenzi ya Mungu ya awali ya Mungu kuwa mwili. Mungu hawi mwili ili kulaani mwanadamu, kufichua mwanadamu akipenda, ama kufanya vitu kuwa vigumu kwa mwanadamu. Hakuna kati ya hayo lililo penzi la awali la Mungu. Kila wakati ambapo Mungu anakuwa mwili, ni kazi isiyo na budi. Ni kwa ajili ya kazi Yake kuu na usimamizi Wake mkuu ndio maana Anafanya hivyo, na si kwa sababu ambazo mwanadamu anafikiria. Mungu anakuja tu duniani Anavyohitajika na kazi Yake, na kila wakati ikiwa lazima. Haji duniani Akiwa na nia ya kuzurura, ila kutekeleza kazi ambayo Anapaswa kufanya. Mbona basi Ajipatie kazi hii ngumu na kujiweka katika hatari kubwa kufanya kazi hii? Mungu anakuwa mwili tu

inapobidi, na kila wakati ikiwa na umuhimu wa kipekee. Kama ingekuwa tu kwa sababu ya kumfanya mwanadamu amuangalie na kufungua macho yao, basi kwa uhakika kabisa, hangekuja kati ya wanadamu kwa kubembeleza. Anakuja duniani kwa usimamizi Wake na kazi Yake kuu, na kuwa na uwezo wa kutwaa wanadamu zaidi. Anakuja kuwakilisha enzi na kumshinda Shetani, na ni katika mwili ndimo Anakuja kumshinda Shetani. Zaidi, Anakuja kuwaongoza binadamu wote katika maisha yao. Haya yote yanahusu uongozi Wake, na yanahusu kazi ya ulimwengu wote. Mungu angekuwa mwili ili tu kumruhusu mwanadamu kuja kuujua mwili Wake na kuyafungua macho ya mwanadamu, basi mbona Hangesafiri kwa kila taifa? Je hili sio jambo la wepesi zaidi? Lakini hakufanya hivyo, badala yake, Akachagua mahali palipofaa pa kuishi na kuanza kazi Aliyopaswa kufanya. Mwili huu pekee ni wa umuhimu mkuu. Anawakilisha enzi nzima, na Anatekeleza kazi ya enzi nzima; Analeta enzi ya zamani kufika tamati na kuikaribisha mpya. Haya yote ni mambo muhimu yanayohusu usimamizi wa Mungu, na ni umuhimu wa hatua ya kazi iliyotekelezwa na Mungu kuja duniani. Wakati ambapo Yesu alikuja duniani, Alizungumza tu maneno kiasi na kutekeleza kazi kiasi; Hakujishughulisha na maisha ya mwanadamu, na Aliondoka baada ya kumaliza kazi Yake. Baada ya Mimi kumaliza kuzungumza na kuyapokeza maneno Yangu kwenu siku hii, nanyi nyote mkishayaelewa, basi hatua hii ya kazi itakuwa imemalizika, haijalishi maisha yenu yatakuwa vipi. Katika siku za usoni, lazima kuwe na wale wa kuendelea hatua hii ya kazi na kufanya kazi kwa mujibu wa maneno haya duniani; kisha kazi ya mwanadamu na ujenzi wa mwanadamu utanza. Lakini sasa, ni kazi ya Mungu tu kutimiza huduma Yake na kumaliza hatua ya kazi. Mungu hufanya kazi kwa njia isiyo sawa na ya mwanadamu. Mwanadamu hupenda mikusanyiko na mabaraza, na huthamini sana utaratibu. Mungu huchukia sana mikusanyiko na mikutano ya mwanadamu. Mungu huzungumza na kunena na mwanadamu visivyo rasmi; hii ni kazi ya Mungu, ambayo ni iliyokombolewa isivyo kawaida na pia hukuweka wewe huru. Hata hivyo, Nachukia zaidi kukusanyika nanyi, na Mimi siwezi kuzoea maisha yaliyoshurutishwa sana kama yenu. Mimi huziona sheria kuwa za kuchukiza sana; hizo humzuia mwanadamu kiasi cha kumfanya mwanadamu aogope kuanza kutenda, aogope kuzungumza, na aogope kuimba, na macho yake hukodolewa kwako moja kwa moja. Nachukia zaidi namna yenu ya mikusanyiko na mikutano mikubwa. Sitamani kabisa kukusanyika nanyi kwa njia hii, kwani njia hii ya kuishi humfanya mtu ahisi amewekewa mipaka na mnafuata utaratibu mwingi sana na sheria nyingi sana. Mngeruhusiwa kuwaongoza wanadamu mngewaongoza wote ndani ya miliki ya sheria na wanadamu hawangekuwa na njia ya kuziacha sheria chini ya uongozi wenu, na badala yake maana ya udini ingekuwa kali sana milele, na desturi za mwanadamu kuongezeka kwa idadi kubwa zaidi. Wanadamu wengine huendelea kuzungumza na kunena wakati ambapo wanakusanyika na hawahisi uchovu kamwe, ilhali wengine wanaweza kuendelea kunena kwa siku nyingi. Hii yote inafikiriwa kuwa mikusanyiko mikubwa na mikutano ya mwanadamu; haina uhusiano wowote na maisha ya kula

na kunywa, ya kufurahia, au ya maisha roho huwekwa huru. Hii yote ni mikutano! Mikutano yenu ya mfanyakazi mshiriki, na vilevile mikusanyiko mikubwa na midogo, yote inanichukiza Mimi, na Sijawahi kuwa na hamu nayo. Hii ni kanuni ambayo Nafanyia kazi; Siko radhi kuhubiri wakati wa mikusanyiko, wala Siko radhi kutangaza chochote kwa watu wote, sembuse kuitisha mkutano wa ninyi nyote kwa siku chache za mkutano maalumu. Sioni likiwa la kupendeza kwenu nyote kukusanyika pamoja kwa kufaa; Nachukia kabisa kuwaona ninyi mkiishi ndani ya mipaka ya utaratibu wowote, aidha, Siko radhi kushiriki katika utaratibu wenu wowote kama huo. Kadri mnavyofanya hivyo, ndivyo Ninavyoiona kuwa ya kuchukiza zaidi. Sina hamu hata kidogo na utaratibu na sheria zenu; haijalishi mnavifanya kwa jinsi nzuri iliyoje, Nayaona yote kuwa ya kuchukiza. Sio kwamba mipango yenu ni isiyofaa au kwamba ninyi ni duni sana; ni kwamba Nachukia sana mwenendo wenu wa kuishi, na zaidi ya hayo, Mimi siwezi kuuzoea. Ninyi hamwelewi kabisa kazi Ninayotaka kufanya. Kipindi hicho, wakati ambapo Yesu alitekeleza kazi Yake mahali fulani na kisha Akamaliza kuhubiri mahubiri, Angewaongoza wanafunzi Wake na kuondoka katika mji huo; Akiondoka kati ya wanadamu, na kuwaongoza wanafunzi wake wachache wapendwa na kuzungumza nao kuhusu njia walizopaswa kuelewa. Alifanya kazi kila mara kwa njia hiyo. Kazi Yake kati ya umma ya jumla ilikuwa nadra. Kulingana na kile mnachotaka kutoka Kwake, Mungu aliyepata mwili hapaswi kuwa na maisha ya mwanadamu wa kawaida; lazima Aitekeleze kazi Yake, na lazima Azungumze, kama Anaketi, Anasimama, au kutembea. Lazima Afanya kazi nyakati zote na Hawezi kukoma “kukimbia”, la sivyo Anazembea katika majukumu Yake. Je, mahitaji haya ya mwanadamu ni kwa mujibu wa akili ya mwanadamu? Uadilifu wenu uko wapi? Je, hamtaki mengi kupita kiasi? Kazi Yangu inahitaji kuchunguzwa na wewe? Je, Nakuhitaji wewe kuangalia Ninapotimiza huduma Yangu? Najua vizuri kazi Ninayopaswa kufanya na wakati ambapo Napaswa kuifanya; Sihitaji kuingilia kutoka kwa wengine. Labda inaweza kuonekana kwako kana kwamba Sijafanya mengi, lakini kufikia wakati huo kazi Yangu tayari imefika mwisho. Chukueni mfano wa maneno ya Yesu katika Injili Nne. Hayo vilevile hayakuwa na mipaka? Wakati huo, Yesu aliingia katika sinagogi na kuhubiri mahubiri; Alikuwa ameimaliza katika muda usio zaidi ya dakika kadhaa. Baada ya Yeye kumaliza kunena, Aliwaongoza wanafunzi Wake ndani ya mashua na Akaondoka bila maelezo yoyote. Sanasana, wale waliokuwa ndani ya sinagogi walijadiliana miongoni mwao wenyewe, na jambo hilo halikumhusu Yesu tena. Mungu alitekeleza tu kazi ambayo Alipaswa kuifanya, na sio zaidi. Siku hizi, wengi huniomba Ninene na kuzungumza mengi zaidi, angalau kwa masaa kadhaa kwa siku. Kama mwonavyo, Mungu huacha kuwa Mungu isipokuwa Azungumze, na ni Yule anayezungumza tu ni Mungu. Ninyi nyote ni vipofu! Nyote ni katili! Nyote ni vitu visivyojua visivyo na hisi! Mna fikira nyingi sana! Madai yenu hupita mipaka! Ninyi ni wasio na utu! Hamwelewi kabisa Mungu ni nini! Ninyi huamini kwamba wazungumzaji na wasemi wote ni Mungu, kwamba yeyote ambaye yuko radhi

kuwapa ninyi maneno ni baba yenu. Niambieni, je, ninyi nyote mlio na maumbo “yaliyoumbwa vizuri” na sura “ya ajabu” bado mna hata sehemu kidogo ya hisi? Je, mnajua sasa jua la mbinguni! Kila mmoja wenu ni kama maofisa wapotovu na wenye uchoyo, kwa hiyo mwawezaje kuona maana? Mwawezaje kutambua kati ya mema na mabaya? Nimewapa ninyi mengi sana, lakini ni wangapi miongoni mwenu wamezingatia? Nani anaweza kulipata kwa ukamilifu? Ninyi hamjui ni nani alifungua njia ambayo kwayo mnatembea siku hii, kwa hiyo ninyi huendelea kunidai Mimi, mkifanya madai yasiyo na maana kutoka Kwangu. Je, nyuso zenu hazijabadilika kwa sababu ya aibu? Sijazungumza mengi? Je, Sijafanya mengi? Ni nani miongoni mwenu anaweza kweli kuyatunza maneno Yangu kama hazina? Ninyi hunisifu mno katika kuwepo Kwangu, lakini hudanganya na kulaghai bila Mimi kujua! Matendo yenu ni yenye kustahili dharau sana na ya kuchukiza! Najua kwamba ninyi huniambia Mimi nizungumze na kufanya kazi ili muweze kushibisha macho yenu na kupanua uzoefu wenu tu, sio kuyageuza maisha yenu. Ni mangapi ambayo Nimenena kwenu tayari? Maisha yenu yangukuwa yamebadilika kitambo sana, kwa hiyo mbona mnaendelea kurudia hali mbaya leo? Yaweza kuwa kwamba maneno Yangu yameibwa kutoka kwenu kwa hivyo hamkuyapokea? Kusema kweli, Sitamani kusema zaidi kwa walioharibika tabia namna hivyo kama ninyi. Haileti manufaa! Siko radhi kufanya kazi isiyoleta manufaa hivyo! Ninye mnataka tu kupanua uzoefu wenu au kuyashibisha macho yenu, sio kupata uzima! Nyote mnajidanganya wenyewe! Nawauliza, ni mangapi kati ya yale Niliyowazungumzia ana kwa ana yametiwa katika vitendo na ninyi? Yote mfanyayo ni ulaghai wa kudanganya! Nachukia sana wale miongoni mwenu wanaofurahia kutazama, na Nauona udadisi wenu kuwa wa kuchukiza kabisa. Kama hamko hapa kuitafuta njia ya kweli au kuwa na kiu ya ukweli, basi ninyi ni wale Ninaowachukia sana! Najua kwamba ninyi hunisikiliza tu ili kuridhisha udadisi wenu au kutimiza mojawapo ya shauku yenu. Hamna wazo la kutafuta kuweko kwa ukweli au kuchunguza kuingia katika njia sahihi ya uzima; matakwa haya hayako miongoni mwenu kabisa. Ninyi humchukulia tu Mungu kuwa mtu anayechezewa wa kuchunguza na kustahi. Moyo wenu unaotafuta uzima ni mdogo sana, ilhali shauku yenu ya udadisi sio! Kuzungumza kwa watu kama hao kuhusu njia ya uzima ni kimsingi kuzungumza na kitu kisichokuwepo; ingekuwa heri kutozungumza! Hebu Niwaambie: Kama mnatazamia tu kuijaza tupu iliyo ndani ya moyo wenu, basi heri msije Kwangu! Mnapaswa kuyalenga maisha yenu! Msijidanganye! Heri msichukulie udadisi wenu kama msingi wa ufuatiliaji wenu wa maisha, au kuutumia kama kisingizio cha kuniomba Mimi kuzungumza na ninyi. Huu wote ni ulaghai, ambao kwao ninyi ni mabingwa! Nakuuliza tena: Ni kiasi gani cha yale ambayo Nimekwambia uingie ndani umefanya kwa kweli? Je, wajua yote ambayo Nimenena kwako? Umetia katika vitendo yote ambayo Nimenena kwako.

Kazi ya kila enzi huanzishwa na Mungu Mwenyewe, lakini unapaswa kujua kwamba licha

ya kazi yoyote ya Mungu, Yeye haji kuanzisha muungano au kufanya mikutano yoyote halisi au kuanzisha makundi ya aina yoyote kwa ajili yenu. Yeye huja tu kufanya kazi Anayopaswa kufanya. Kazi Yake haizuiliwi na mwanadamu yeyote. Yeye hufanya kazi Yake vile Anavyopenda; haijalishi kile mwanadamu anajua au kufikiri, Yeye hutilia maanani katika kutekeleza kazi Yake. Tangu kuumbwa kwa dunia, kumekuwa na hatua tatu za kazi; kutoka kwa Yehova mpaka kwa Yesu, na kutoka kwa Enzi ya Sheria mpaka kwa Enzi ya Neema, Mungu hajawahi kuitisha mkutano halisi kwa mwanadamu, wala hajawahi kuwakusanya wanadamu wote pamoja kufanya mkutano halisi wa ulimwengu ili kupanua kazi Yake. Yeye hufanya tu kazi ya mwanzo wa enzi nzima wakati muda na wakati na mahali uko sawa, na kupitia kwa hili Anaikaribisha enzi ili kuwaongoza wanadamu katika maisha yao. Mikutano halisi ni mikutano ya wanadamu; kuwakusanya watu pamoja kusherehekea siku kuu katika kazi za mwanadamu. Mungu hasherehekei siku kuu na, zaidi ya hayo, Anachukizwa nazo; Yeye haitishi mikutano halisi na zaidi ya hayo Anachukizwa nayo. Sasa lazima uelewe ni nini hasa kazi ya Mungu mwenye mwili.

Fumbo la Kupata Mwili (4)

Mnapaswa kujua kuhusu hadithi ya ndani na uumbaji wa Biblia. Ufahamu huu haushikiliwi na wale ambao hawajakubali kazi mpya ya Mungu. Wao hawajui. Ikiwa ungewaelezea, mambo haya ya kiini, wasingekuwa tena wenye kushikilia sana elimu ya vitabuni na sheria kuhusu Biblia na wewe. Wao huchunguza kwa uthabiti kile ambacho kimetabiriwa: Kauli hii imeshatimia? Kauli ile imeshatimia? Kukubali kwao injili ni kwa mujibu wa Biblia, na wao huhubiri injili kulingana na Biblia. Wao huyategemea maneno ya Biblia kumwamini Mungu; bila Biblia, wao hawatamwamini Mungu. Hii ndiyo njia ambayo wao huishi, kuichunguza Biblia hivyo. Wakati ambapo wao huchunguza Biblia tena na kukuuliza wewe kuhusu ufafanuzi, unasema, “Kwanza, hebu tusithibitishe kila kauli. Badala yake, hebu tuangalie vile Roho Mtakatifu hufanya kazi. Hebu tulinganishe njia tunayoitembea dhidi ya ukweli ili tuone kama njia tunayoitembea kweli ni kazi ya Roho Mtakatifu, na hebu tutumie kazi ya Roho Mtakatifu kuangalia kwa makini kama njia kama hiyo ni sahihi. Kuhusu kama kauli hii au kauli ile imeshatimia, sisi binadamu hatupaswi kuingilia. Ni bora kwetu badala yake kuzungumza kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu na kazi ya karibuni zaidi ambayo Mungu amekuwa akifanya.” Unabii katika Biblia ni maneno ya Mungu yaliyopitishwa wakati huo na manabii na maneno yaliyoandikwa na watu waliotumiwa na Mungu, baada ya kutiwa msukumo; ni Mungu Mwenyewe tu ndiye anaweza kueleza maneno hayo, Roho Mtakatifu pekee ndiye anaweza kutambulisha maana ya maneno hayo, na Mungu Mwenyewe tu ndiye anaweza kuivunja mihuri saba na kukifungua kitabu. Unasema: “Wewe si Mungu, na wala Mimi si Mungu, kwa hiyo nani anathubutu kueleza kwa hiari maneno ya Mungu? Je, wewe unathubutu kueleza maneno hayo?”

Hata kama manabii Yeremia, Yohana na Eliya wangukuwa hapa, hawangethubutu, kwani wao si Mwanakondoo. Ni Mwanakondoo pekee ndiye anaweza kuivunja mihuri saba na kufungua kitabu, na hakuna mwingine awezaye kuyaeleza maneno Yake. Sithubutu kunyang'anya jina la Mungu, seuze kujaribu kuyaeleza maneno ya Mungu. Naweza tu kuwa yule ambaye humtii Mungu. Je, wewe ni Mungu? Hakuna viumbe wa Mungu ambao huthubutu kufungua kitabu au kuyafafanua maneno hayo, na hivyo Sithubutu kuyaeleza pia. Ni bora usijaribu kuyaeleza. Hakuna kati yetu anayepaswa kujaribu kuyaeleza. Hebu tuzungumze kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu; hili ndilo mwanadamu anaweza kufanya. Najua machache kuhusu kazi ya Yehova na Yesu, lakini kwa vile Sina uzoefu Wangu binafsi na kazi hiyo, Naweza tu kuizungumzia kwa kiasi kidogo. Kuhusu maneno yaliyonenwa na Isaya au Yesu wakati huo, Sitafanya ufafanuzi. Sijifunzi Biblia, lakini badala yake Mimi hufuata kazi ya sasa ya Mungu. Wewe kwa kweli unaichukulia Biblia kuwa kitabu kidogo, lakini siyo kweli kwamba kinaweza tu kufunguliwa na Mwanakondoo. Isipokuwa Mwanakondoo, nani mwingine anaweza kukifungua? Wewe si Mwanakondoo, na wala Mimi sithubutu kudai kuwa Mungu Mwenyewe, kwa hiyo hebu tusichambue au kuichunguza Biblia. Bora kujadili kazi ambayo hufanywa na Roho Mtakatifu, yaani, kazi ya sasa ambayo hufanywa na Mungu Mwenyewe. Hebu tuangalie kanuni ambazo kwazo Mungu hufanya kazi ni zipi na kiini cha kazi Yake ni kipi, kisha tuyaangalie kwa makini dhidi ya hayo kuona kama njia tunayotembea siku hii ni ya kweli. Hebu tulinganishe na hili kama kiwango.” Kama ninyi huhubiri injili, hasa kwa wale walio katika ulimwengu wa kidini, lazima muelewe Biblia na muwe na ujuzi wa hadithi yake ya ndani, la sivyo, hutaweza kuhubiri injili. Mara tu unapopata utambuzi wa taswira kubwa, usiyachunguze maneno ya Biblia yaliyopitwa na wakati, na zungumza tu kuhusu kazi ya Mungu na ukweli wa maisha, kisha utaweza kuwapata wale wanaotafuta kwa roho ya kweli.

Mnafaa kuelewa kazi ya Yehova, sheria Alizoweka, na kanuni ambazo kwazo Aliyaongoza maisha ya mwanadamu, yaliyomo kwenye kazi Aliyofanya katika Enzi ya Sheria, umuhimu wa Yeye kuziweka sheria Zake, umuhimu wa kazi Yake katika Enzi ya Neema, na kazi anayofanya Mungu kwenye awamu hii ya mwisho. Hatua ya kwanza ni kazi ya Enzi ya Sheria, hatua ya pili ni kazi ya Enzi ya Neema, na hatua ya tatu ni kazi ya siku za mwisho. Lazima muelewe awamu hizi za kazi ya Mungu. Tangu mwanzo hadi mwisho, kuna hatua tatu kwa jumla. Ni nini kiini cha kila hatua ya kazi? Ni hatua ngapi hutekelezwa katika kazi ya mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita? Kila hatua hutekelezwa vipi, na kwa nini kila mojawapo hutekelezwa kwa njia hii? Haya yote ni maswali ya maana sana. Kazi ya kila enzi ni wakilishi. Yehova alitekeleza kazi gani? Mbona Alifanya hivyo? Mbona Aliitwa Yehova? Yesu alitekeleza kazi gani katika Enzi ya Neema, na Alifanyaje hivyo? Ni vipengele vipi vya tabia ya Mungu huwakilishwa na kila hatua ya kazi na kila enzi? Ni hali zipi za tabia Yake zilijitokeza katika Enzi ya Sheria? Na ni vipi

vilivyoonyeshwa katika Enzi ya Neema? Na ni vipi katika enzi ya mwisho? Haya maswali halisi ni yale ambayo ni lazima myaelewe. Tabia yote ya Mungu imefichuliwa katika mpango wote wa uongozi wa miaka elfu sita. Haikufichuliwa tu katika Enzi ya Neema, ni katika Enzi ya Sheria tu, na zaidi ya hayo, ni katika wakati huu wa siku za mwisho. Kazi iliyofanywa katika siku za mwisho inawakilisha hukumu, ghadhabu na kuadibu. Kazi ifanywayo katika siku za mwisho haiwezi kuwekwa mbadala wa kazi ya Enzi ya Sheria ama ile ya Enzi ya Neema. Ingawa, hatua zote tatu zinaungana kuwa kitu kimoja na yote ni kazi iliyofanywa na Mungu mmoja. Kawaida, utekelezaji wa kazi hizi umegawanyishwa katika enzi tofauti. Kazi iliyofanywa katika siku za mwisho inaleta kila kitu mpaka tamati; ile iliyofanywa katika Enzi ya Sheria ilikuwa ya mwanzo; na ile iliyofanywa katika Enzi ya Neema ilikuwa ya ukombozi. Na kuhusu maono ya kazi katika mpango wote wa usimamizi wa miaka elfu sita, hakuna anayeweza kupata ufahamu au kuelewa. Maono kama hayo yamebaki kuwa mafumbo kila wakati. Katika siku za mwisho, kazi ya neno pekee inafanyika ili kuukaribisha Wakati wa Ufalme lakini haiwakilishi enzi zile zingine. Siku za mwisho sio zaidi ya siku za mwisho na sio zaidi ya Enzi ya Ufalme, na haziwakilishi Enzi ya Neema au Enzi ya Sheria. Siku za mwisho ni wakati ambapo kazi zote ndani ya mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita inafichuliwa kwenu. Mafumbo kama hayo hayawezi kufichuliwa na mwanadamu yeyote. Haijalishi mwanadamu ana maarifa makubwa ya Biblia vipi, yanabaki tu kuwa maneno na si kitu zaidi, kwani mwanadamu haelewi kiini cha Biblia. Mwanadamu anaposoma Biblia, anaweza kupokea baadhi ya ukweli, kueleza baadhi ya maneno ama kuchunguza vifungu maarufu na nukuu, lakini hatawahi kuwa na uwezo wa kunasua maana iliyoko katika maneno hayo, kwani yote aonayo mwanadamu ni maneno yaliyokufa pekee, sio matendo ya kazi ya Yehova na Yesu, na mwanadamu hawezi kufumbua mafumbo ya kazi ya aina hiyo. Kwa hivyo, fumbo la mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita ni fumbo kuu, iliyofichwa zaidi na isiyoshawishika kwa mwanadamu. Hakuna anayeweza kuelewa moja kwa moja mapenzi ya Mungu, ama, Mungu Mwenyewe aeleze na kumfichulia mwanadamu, vinginevyo, yatabaki kuwa mafumbo milele kwa mwanadamu na kubaki mafumbo yaliyofungwa milele. Usiwajali wale walio katika ulimwengu wa kidini; kama hamngeambiwa leo, pia nyinyi hamngeweza kuelewa. Kazi hii ya miaka elfu sita ni ya fumbo zaidi kuliko unabii wote wa manabii. Ni fumbo kuu zaidi tangu uumbaji, na hakuna nabii wa awali ambaye amewahi kuweza kulielewa, kwani fumbo hili hufumbuliwa tu katika enzi ya mwisho na kamwe halijawahi kufichuliwa hapo awali. Mkielewa fumbo hili na muweze kulipokea kwa ukamilifu, wale watu wote wa kidini watahindwa kwa fumbo hili. Hili pekee ndilo kuu zaidi ya maono, lile ambalo mwanadamu hutamani sana kulielewa lakini pia lile ambalo si wazi zaidi kwake. Mlipokuwa katika Enzi ya Neema, hamkujua kazi ambayo ilifanywa na Yesu wala ile ambayo ilifanywa na Yehova. Watu hawakuelewa chochote kuhusu kwa nini Yehova alitangaza sheria, kwa nini Aliwaambia watu wazitii sheria au kwa nini ilikuwa lazima kwa hekalu kujengwa, na sembuse

watu kuelewa kwa nini Waisraeli waliongozwa kutoka Misri hadi jangwani na kisha hadi Kanaani. Ni mpaka siku hii ndipo mambo haya yamefichuliwa.

Kazi katika siku za mwisho ni hatua ya mwisho kati ya hizo tatu. Ni kazi ya enzi nyingine mpya na haiwakilishi kazi ya usimamizi mzima. Mpango wa miaka elfu sita umegawa katika hatua tatu za kazi. Hakuna hatua moja pekee itakayowakilisha kazi ya enzi hizo tatu ila inaweza tu kuwakilisha sehemu moja ya yote. Jina Yehova haliwezi kuwakilisha tabia yote ya Mungu. Ukweli kuwa Alitekeleza kazi katika Enzi ya Sheria sio ushahidi kuwa Mungu Anaweza tu kuwa Mungu chini ya sheria. Yehova alitengeneza sheria kwa mwanadamu na kutoa amri, Akimuuliza mwanadamu ajenge hekalu na madhabahu; kazi Aliyofanya inawakilisha tu Enzi ya Sheria. Kazi Aliyoifanya haidhibitishi kuwa Mungu ni Mungu Anayemwamuru mwanadamu kufuata sheria, Mungu Aliye hekaluni, ama Mungu Aliye mbele ya madhabahu. Haya hayawezi kusemwa. Kazi chini ya sheria inaweza tu kuwakilisha enzi moja. Kwa hivyo, kama Mungu Alifanya kazi katika Enzi ya Sheria pekee, mwanadamu angemfafanua Mungu na kusema, “Mungu ni Mungu Aliye hekaluni. Ili kumtumikia Mungu, lazima tuvae mavazi ya kikuhani na tuingie hekaluni.” Iwapo kazi katika Enzi ya Neema haingetekelezwa na Enzi ya Sheria ingeendelea mpaka wakati huu wa sasa, mwanadamu hangefahamu kuwa Mungu pia ni mwenye huruma na upendo. Iwapo kazi katika Enzi ya Sheria haingefanywa, na badala yake kazi katika Enzi ya Neema pekee, basi yote ambayo mwanadamu angefahamu ni kwamba Mungu Anakomboa tu mwanadamu na kumsamehe dhambi zake. Wangefahamu tu kuwa Yeye ni mtakatifu na asiye na hatia, kwamba Anaweza kujitoa kafara na kusulubishwa kwa ajili ya mwanadamu. Mwanadamu angejua tu kuhusu haya na asiwe na ufahamu wa mambo mengine yoyote. Kwa hivyo kila enzi inawakilisha sehemu moja ya tabia ya Mungu. Enzi ya Sheria inawakilisha vipengele vingine, Enzi ya Neema vipengele vingine na enzi hii vipengele vingine. Tabia ya Mungu inaweza tu kuonekana kwa mchanganyiko wa hatua zote tatu. Ni wakati tu mwanadamu anajua hatua hizi tatu ndipo anaweza kuipokea kikamilifu. Hakuna hatua kati ya hizo tatu ambayo inaweza kuachwa. Utaiona tu tabia ya Mungu kwa ukamilifu wake mara tu utakapozijua hatua hizi tatu za kazi. Ukweli kamba Mungu alikamilisha kazi yake katika Enzi ya Sheria sio ushahidi kwamba Yeye ni Mungu chini ya sheria tu, na ukweli kamba alikamilisha kazi Yake ya ukombozi haimaanishi kuwa Mungu Atamkomboa mwanadamu milele. Hizi zote ni hitimisho zilizofanywa na mwanadamu kuhusu jambo hilo. Enzi ya Neema ikiwa imefika mwisho, huwezi basi kusema kuwa Mungu ni wa msalaba tu na kuwa msalaba pekee unawakilisha wokovu wa Mungu. Ukifanya hivyo, basi utakuwa unamfasili Mungu. Katika hatua hii, Mungu Anafanya zaidi kazi ya Neno, lakini huwezi kusema kuwa Mungu hajawahi kuwa Mwenye huruma kwa mwanadamu na kwamba yote Aliyoleta ni kuadibu na hukumu. Kazi katika siku za mwisho inaonyesha wazi kazi ya Yehova na ile ya Yesu na mafumbo yote yasioeleweka na mwanadamu. Hii inafanywa ili

kuonyesha hatima na mwisho wa binadamu na kukamilisha kazi yote ya wokovu miongoni mwa wanadamu. Hatua hii ya kazi katika siku za mwisho huleta kila kitu kufika mwisho. Mafumbo yote yasiyoeleweka na mwanadamu yanapaswa kufunuliwa ili kumpa mwanadamu ufahamu na kuweza kuelewa kwa kina katika mioyo yao. Hapo tu ndipo wanadamu wataweza kuainishwa kulingana na aina. Baada tu ya mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita kukamilishwa ndipo mwanadamu atapata kuelewa tabia ya Mungu kwa ukamilifu wake, kwani usimamizi Wake utakuwa umefika mwisho. Kwa kuwa mmeipitia kazi ya Mungu katika enzi ya mwisho, tabia ya Mungu ni gani? Je, wewe unathubutu kusema kwamba Mungu ni Mungu ambaye hunena maneno tu? Hungeweza kuthubutu kufanya uamuzi huu. Wengine husema kwamba Mungu ni Mungu ambaye kufunua siri, kwamba Mungu ni Mwanakondoo na Ambaye huvunja mihuri saba. Hakuna ambaye huthubutu kufanya uamuzi huu. Na kuna wengine ambao husema kwamba Mungu ni aliyepata mwili. Hili bado si sahihi. Wengine husema kwamba Mungu mwenye mwili hunena maneno tu na Hafanyi ishara na maajabu. Wala hungeweza kuthubutu kunena kwa njia hii, kwani Yesu alipata mwili na Alifanya ishara na maajabu, kwa hiyo wewe huthubutu kumfafanua Mungu kwa urahisi. Kazi yote iliyofanyika katika mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita imefika mwisho sasa. Ni baada tu ya kazi hii kubainika wazi kwa wanadamu na kutekelezwa miongoni mwa wanadamu ndipo watakapofahamu tabia ya Mungu na kile alichona anacho. Kazi za enzi hizi zitakapokamilika, mafumbo yote yasiyoeleweka na mwanadamu yatakuwa yamebainika, ukweli wote ambao haukuwa unaeleweka utawekwa wazi, na mwanadamu atakuwa ameambiwa njia na hatima ya baadaye. Hii ndio kazi yote inayopaswa kufanyika katika hatua hii. Ingawa njia ambayo mwanadamu hutembea leo pia ni njia ya msalaba na ya kuteseka, kile ambacho mwanadamu wa leo hutenda, hula, hunywa na hufurahia ni tofauti zaidi na yale ya mwanadamu aliyekuwa chini ya sheria na katika Enzi ya Neema. Kinachohitajika kutoka kwa mwanadamu wakati huu sio kama ilivyokuwa kitambo na zaidi sio kama kilichohitajika kutoka kwake katika Enzi ya Sheria. Na ni kipi kilichoulizwa kwa mwanadamu chini ya Sheria Mungu alipokuwa akifanya kazi huko Israeli? Hawakuulizwa chochote zaidi ya kuiheshimu Sabato na Sheria za Yehova. Lakini si hivyo katika wakati huu. Siku ya Sabato, mwanadamu anafanya kazi, hukusanyika na kuomba kama kawaida, na hakuna vizuizi vinavyowekwa. Wale katika Enzi ya Neema ilibidi wabatizwe, na pia zaidi walitarajiwa kufunga, kuvunja mkate, kunywa divai, kufunika vichwa vyao na kuwaoshea wengine miguu yao. Sasa, sheria hizi zimefutwa na mahitaji makuu yanaulizwa kutoka kwa mwanadamu, kwani kazi ya Mungu inazidi kuwa ya kina na kuingia kwa mwanadamu kunafika kiwango cha juu. Zamani, Yesu Aliweka mikono Yake juu ya mwanadamu na kuomba, lakini sasa kwamba kila kitu kimesemwa, kuwekelea mikono kuna maana gani? Maneno pekee yanaweza kupata matokeo. Alipowekelea mikono Yake juu ya mwanadamu hapo awali, ilikuwa ni kwa ajili ya kumbariki na kumponya mwanadamu. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu Alivyofanya kazi wakati

huo, lakini sio hivyo wakati huu. Wakati huu, Roho Mtakatifu Anatumia maneno katika kazi Yake ili kupata matokeo. Ameyafanya maneno Yake wazi kwenu, na mnapaswa tu kuyaweka katika matendo. Maneno Yake ni mapenzi Yake na yanaonyesha kazi Atakayofanya. Kupitia katika maneno Yake, utaweza kuelewa mapenzi Yake na yale ambayo Anauliza upate, na unaweza kuyaweka tu maneno Yake katika matendo moja kwa moja bila haja ya kuwekelea mikono. Wengine wanaweza kusema, “Wekelea mikono Yako juu yangu! Wekelea mikono yako juu yangu ili niweze kupokea baraka zako na kushiriki kwako.” Haya yote ni mazoezi yaliyopitwa na wakati na ambayo yanakataliwa katika wakati huu, kwani enzi zimebadilika. Roho Mtakatifu Anafanya kazi kulingana na enzi, sio tu katika mapenzi Yake ama kulingana na masharti. Enzi zimebadilika, na enzi mpya lazima ilete kazi mpya. Huu ni ukweli wa kila hatua ya kazi, na hivyo kazi Yake haiwezi kurudiwa. Katika Enzi ya Neema, Yesu Alifanya nyingi ya kazi hiyo, kama kuponya magonjwa, kukemea mapepo, kuwekelea mikono Yake juu ya wanadamu, na kumbariki mwanadamu. Hata hivyo, kuendelea kufanya hivyo hakutasaidia chochote katika wakati huu. Roho Mtakatifu Alifanya kazi hivyo katika huo wakati, kwani ilikuwa Enzi ya Neema, na mwanadamu alipewa neema ya kutosha ili afurahie. Mwanadamu hakuhitajika kulipa gharama yoyote na angepokea neema mradi tu angekuwa na imani. Kila mtu alitendewa kwa neema kubwa. Sasa, enzi imebadilika, na kazi ya Mungu imeendelea zaidi; kupitia kuadibu na hukumu Yake, uasi wa mwanadamu na vitu vichafu katika mwanadamu vitatupiliwa mbali. Jinsi ilivyokuwa hatua ya wokovu, ilimbidi Mungu kufanya kazi hiyo, Akimwonyesha mwanadamu neema ya kutosha ili mwanadamu afurahie, ili Amkomboe mwanadamu kutoka kwa dhambi, na kwa neema, amsamehe mwanadamu dhambi zake. Hatua hii ya sasa ni ya kufichua udhalimu ulio ndani ya mwanadamu kwa njia ya kuadibu, hukumu, kupigwa na maneno, na vile vile nidhamu na ufunuo wa maneno, ili baadaye binadamu waweze kuokolewa. Hii ni kazi ya undani zaidi kuliko ukombozi. Katika Enzi ya Neema, mwanadamu alifurahia neema ya kutosha na amezoea neema hii, kwa hivyo sio ya kufurahiwa na mwanadamu tena. Kazi kama hii imepitwa na wakati sasa na haitafanyika tena. Sasa, mwanadamu anaokolewa kupitia hukumu ya neno. Baada ya mwanadamu kuhukumiwa, kuadibiwa na kusafishwa, tabia yake basi inabadilika. Je sio kwa sababu ya maneno ambayo Nimenena? Kila hatua ya kazi inafanywa kulingana na maendeleo ya binadamu wote na kwa enzi. Kazi yote ina umuhimu wake; inafanywa kwa ajili ya wokovu wa mwisho, ili binadamu awe na hatima nzuri baadaye, na kwa binadamu kuainishwa kulingana na aina mwishowe.

Kazi katika siku za mwisho ni kunena maneno. Mabadiliko makuu yanaweza kusababishwa kwa watu kupitia katika maneno hayo. Mabadiliko yanayosababishwa sasa kwa watu hawa kwa sababu ya kukubali maneno haya ni makubwa kuliko yale ya watu katika Enzi ya Neema kwa kukubali ishara na maajabu hayo. Kwani, katika Enzi ya Neema, mapepo yaliondoka kutoka kwa

mwanadamu kwa kuwekewa mikono na maombi, lakini tabia potovu ndani ya mwanadamu ilibaki. Mwanadamu aliponywa magonjwa na kusamehewa dhambi zake, lakini kazi ya jinsi tabia potovu za kishetani katika mwanadamu haikutupiliwa mbali na bado iko ndani yake. Mwanadamu aliokolewa na kusamehewa dhambi zake kwa imani yake, lakini asili ya dhambi ya mwanadamu haikuchukuliwa na ikabaki naye. Dhambi za mwanadamu zilisamehewa kupitia mwili wa Mungu mwenye mwili, lakini hili halikumaanisha kuwa mwanadamu hakuwa na dhambi ndani yake. Dhambi za mwanadamu zingesamehewa kupitia sadaka ya dhambi, lakini mwanadamu hajaweza kutatua suala la vipi hangeweza kutenda dhambi na vile asili Yake ya dhambi ingetupiliwa mbali kabisa na kubadilishwa. Dhambi za mwanadamu zilisamehewa kwa sababu ya kazi ya Mungu ya kusulubiwa, lakini mwanadamu akaendelea kuishi katika tabia yake potovu ya zamani ya kishetani. Hivyo, mwanadamu lazima aokolewe kabisa kutoka kwa tabia potovu za kishetani ili asili ya dhambi ya mwanadamu itupiliwe mbali kabisa na isirudi tena, hivyo kukubali tabia ya mwanadamu kubadilika. Hii inampasa mwanadamu kuelewa njia ya kukua katika maisha, njia ya maisha, na jinsi ya kubadilisha tabia yake. Inamhitaji pia mwanadamu kutenda kulingana na njia hii ili tabia ya mwanadamu iweze kubadilika hatua kwa hatua na aishi chini ya nuru inayong'aa, na aweze kufanya mambo yote kulingana na mapenzi ya Mungu, atupilie mbali tabia potovu za kishetani, na kutoka kwa ushawishi wa Shetani wa giza, hivyo kutoka kabisa katika dhambi. Ni hapo tu ndipo mwanadamu atapokea wokovu kamili. Yesu Alipokuwa Akifanya kazi Yake, maarifa ya mwanadamu juu Yake yalikuwa bado hayakuwa bayana na hayakuwa wazi. Mwanadamu aliamini kila wakati kuwa Alikuwa Mwana wa Daudi na kumtangaza kuwa nabii mkuu na Bwana mwema Aliyezikomboa dhambi za mwanadamu. Wengine, wakiwa na msingi wa imani, wakaponywa tu kwa kugusa vazi Lake; vipofu wakaona na hata wafu kurejeshwa katika uhai. Hata hivyo, mwanadamu hangeweza kutambua tabia potovu za kishetani zilizokita mizizi ndani yake na pia mwanadamu hakujua jinsi ya kuitoa. Mwanadamu alipokea neema nyingi, kama amani na furaha ya mwili, baraka ya familia nzima juu ya imani ya mmoja, na kuponywa magonjwa, na mengine mengi. Yaliyobaki ni matendo mema ya mwanadamu na kuonekana kwa kiungu; kama mtu angeishi katika huo msingi, angechukuliwa kama muumini mzuri. Waumini hao tu ndio wangeingia mbinguni baada ya kifo, ambayo ilimaanisha kuwa walikuwa wameokolewa. Lakini katika maisha yao, hawakuelewa kamwe njia ya maisha. Walitenda tu dhambi, na kisha kukiri kila wakati bila njia yoyote ya kubadili tabia yao; hii ndiyo ilikuwa hali ya mwanadamu katika Enzi ya Neema. Je mwanadamu amepokea wokovu kamili? La! Kwa hivyo, hatua ilipokamilika, bado kuna kazi ya hukumu na kuadibu. Hatua hii ni ya kumfanya mwanadamu awea safi kupitia neno, na hivyo kumpa njia ya kufuata. Hatua hii haingekuwa na matunda ama ya maana kama ingeendelea na kukemea mapopo, kwani msingi wa dhambi wa mwanadamu haungetupwa mbali na mwanadamu angekoma tu baada ya msamaha wa dhambi. Kupitia kwa sadaka ya dhambi,

mwanadamu amesamehewa dhambi zake, kwani kazi ya kusulubisha imefika mwisho na Mungu Ametawala juu ya Shetani. Lakini tabia potovu ya wanadamu bado imebaki ndani yao na mwanadamu anaweza kutenda dhambi na kumpinga Mungu; Mungu hajampata mwanadamu. Hiyo ndio sababu katika hatua hii ya kazi Mungu Anatumia neno kutangaza tabia potovu ya mwanadamu na kumuuliza mwanadamu kutenda kulingana na njia sahihi. Hatua hii ni ya maana zaidi kuliko zile za awali na pia yenye mafanikio zaidi, kwani wakati huu ni neno ambalo linatoa maisha moja kwa moja kwa mwanadamu na linawezesha tabia ya mwanadamu kubadilishwa kabisa; ni hatua ya kazi ya uhakika kabisa. Kwa hivyo, Mungu kupata mwili katika siku za mwisho imekamilisha umuhimu wa Mungu kupata mwili wa Mungu na kukamilisha usimamizi wa Mungu katika mpango wa kuokoa mwanadamu.

Wokovu wa Mungu kwa mwanadamu haufanywi moja kwa moja kupitia njia ya Roho ama kama Roho, kwani Roho Wake hawezi kuguzwa ama kuonekana na mwanadamu, na hawezi kukaribiwa na mwanadamu. Kama Angejaribu kumwokoa mwanadamu moja kwa moja kwa njia ya Roho, mwanadamu hangeweza kupokea wokovu Wake. Na kama sio Mungu kuvalia umbo la nje la mwanadamu aliyeumbwa, mwanadamu hawangeweza kupokea wokovu huu. Kwani mwanadamu hawezi kumkaribia kwa njia yoyote ile, zaidi kama jinsi hakuna anayeweza kukaribia wingu la Yehova. Ni kwa kuwa mwanadamu wa kuumbwa tu, hivyo ni kusema, kuliweka neno Lake katika mwili Atakaogeukana kuwa, ndio ataweza kulifanya neno yeye Mwenyewe ndani ya wale wote wanaomfuata. Hapo ndipo mwanadamu atasikia mwenyewe neno Lake, kuona neno Lake, na kupokea neno Lake, kisha kupitia hili aokolewe kamili. Kama Mungu hangegeuka na kupata mwili, hakuna mtu mwenye mwili ambaye angepokea wokovu huo mkuu, wala hakuna mtu hata mmoja ambaye angeokolewa. Kama Roho wa Mungu angefanya kazi moja kwa moja kati ya mwanadamu, mwanadamu angepigwa ama kubebwa kabisa kama mfungwa na Shetani kwani mwanadamu hawezi kushirikiana na Mungu. Kupata mwili mara ya kwanza kulikuwa kumkomboa mwanadamu kutoka katika dhambi kupitia mwili wa Yesu, hivyo, Aliokoa mwanadamu kutoka kwa msalaba, lakini tabia potovu ya kishetani ilibaki ndani ya mwanadamu. Kupata mwili mara ya pili si kwa ajili ya kuhudumu tena kama sadaka ya dhambi ila ni kuwaokoa kamilifu wale waliokombolewa kutoka kwa dhambi. Hii inafanyika ili wale waliosamehewa wakombolewe kutoka kwa dhambi zao, na kufanywa safi kabisa, na kupata mabadiliko ya tabia, hivyo kujikwamua kutoka kwa ushawishi wa Shetani wa giza na kurudi mbele za kiti cha enzi cha Mungu. Hivyo tu ndivyo mwanadamu ataweza kutakaswa kikamilifu. Mungu Alianza kazi ya wokovu katika Enzi ya Neema baada ya Enzi ya Sheria kufika mwisho. Ni mpaka siku za mwisho tu ambapo Mungu Ametakasa binadamu kikamilifu kwa kufanya kazi ya hukumu na kuadibu mwanadamu kwa kuwa muasi, ndipo Mungu atakamilisha kazi Yake ya wokovu na kupumzika. Kwa hivyo, katika hatua tatu za kazi,

ni mara mbili tu ndipo Mungu amekuwa mwili ili kufanya kazi Yake kati ya mwanadamu Mwenyewe. Hiyo ni kwa sababu moja tu kati ya hatua tatu za kazi ni kuwaongoza wanadamu katika maisha yao, ilhali zingine mbili ni kazi ya wokovu. Mungu Anapokuwa mwili tu ndipo Atakapoishi pamoja na mwanadamu, kuzoea mateso ya dunia, na kuishi katika mwili wa kawaida. Ni kwa namna hii tu ndipo Ataweza kuwapa wanadamu njia ya vitendo wanayohitaji kama viumbe. Mwanadamu anapokea wokovu kamili kutoka kwa Mungu kwa sababu ya Mungu mwenye mwili, sio moja kwa moja kutoka kwa maombi yao kwenda mbinguni. Kwani mwanadamu ni mwenye mwili; mwanadamu hawezi kuona Roho wa Mungu na pia kutoweza kumkaribia. Kile tu mwanadamu anaweza kushiriki ni mwili wa Mungu; kupitia Yeye tu ndipo mwanadamu ataweza kuelewa njia zote, na ukweli wote, na kupokea wokovu kamili. Kupatikana kwa mwili mara ya pili kunatosha kumaliza dhambi za mwanadamu na kumtakasa mwanadamu. Hivyo, kupatikana kwa mwili mara ya pili kutafikisha tamati kazi yote ya Mungu mwenye mwili na kukamilisha umuhimu wa Mungu kupata mwili. Baada ya hapo, kazi ya Mungu mwenye mwili itakuwa imefika mwisho kabisa. Baada ya kupata mwili mara ya pili, hatakuwa mwili tena kwa kazi Yake. Kwani usimamizi Wake wote utakuwa umefika mwisho. Katika siku za mwisho, mwili Wake utakuwa umepata watu Wake teule kabisa, na yote mwanadamu katika siku za mwisho watakuwa wameainishwa kulingana na aina. Hatafanya kazi ya wokovu tena, wala Hatarudi kuwa mwili ili kutekeleza kazi yoyote. Katika kazi ya siku za mwisho, neno ni kubwa zaidi ya udhihirisho wa ishara na maajabu, na mamlaka ya neno yanashinda yale ya ishara na maajabu. Neno linaweka wazi tabia zote potovu katika moyo wa mwanadamu. Huwezi kutambua binafsi wewe mwenyewe. Yatakapofunuliwa kwako kupitia kwa neno, utakuja kujua mwenyewe; hutaweza kuyakataa, na utashawishika kikamilifu. Je haya si mamlaka ya neno? Haya ndiyo matokeo yanayopatikana kwa kazi ya wakati huu ya neno. Kwa hivyo, mwanadamu hawezi kuokolewa kikamilifu kutoka kwa dhambi zake kwa kuponya magonjwa na kukemea mapepo na hawezi kufanywa mkamilifu kabisa kwa udhihirisho wa ishara na maajabu. Mamlaka ya kuponya na kukemea mapepo yanapatia mwanadamu neema tu, lakini mwili wa mwanadamu bado ni wa Shetani na tabia potovu za kishetani zitabaki ndani ya mwanadamu. Kwa maneno mengine, yale ambayo hayajatakaswa bado inahusu dhambi na uchafu. Ni baada tu ya mwanadamu kufanywa safi kupitia kwa maneno ndipo mwanadamu atakapopatwa na Mungu na kutakaswa. Wakati mapepo yalikemewa kutoka kwa mwanadamu na alikombolewa, hii ilimaanisha tu kwamba alipokonywa kutoka kwa mikono ya Shetani na kurudishwa kwa Mungu. Hata hivyo, hajafanywa msafi ama kubadilishwa na Mungu, anabaki kama mpotovu. Ndani ya mwanadamu bado kuna uchafu, pingamizi na uasi; mwanadamu amerudi tu kwa Mungu kupitia kwa ukombozi Wake, lakini mwanadamu hana maarifa hata kidogo kumhusu Mungu na bado anaweza kumpinga na kumsaliti. Kabla ya mwanadamu kukombolewa, sumu nyingi ya Shetani ilikuwa imepandwa ndani yake tayari. Baada ya miaka mingi ya upotovu wa Shetani,

mwanadamu tayari ana asili ndani yake inayompinga Mungu. Hivyo, mwanadamu atakapokombolewa, hakitakuwa kitu kingine ila ni ukombozi, ambapo mwanadamu ananunuliwa kwa gharama kuu, lakini asili ya sumu ndani yake haijaondolewa. Mwanadamu ambaye amechafuliwa lazima apitie mabadiliko kabla ya kuwa wa kustahili kumtumikia Mungu. Kupitia kazi hii ya kuadibu na hukumu, mwanadamu atakuja kujua hali yake kamili ya uchafu na upotovu ndani Yake, na ataweza kubadilika kabisa na kuwa msafi. Ni hivi tu ndivyo mwanadamu ataweza kustahili kurudi katika kiti cha enzi cha Mungu. Kazi yote ifanywayo siku hii ya leo ni ili mwanadamu afanywe msafi na kubadilika; kupitia hukumu na kuadibiwa na neno, na pia kutakaswa, mwanadamu anaweza kuacha nje upotovu wake na kufanywa safi. Badala ya kuichukua hatua hii ya kazi kuwa ile ya wokovu, itafaa zaidi kusema kuwa ni kazi ya utakaso. Kwa kweli hatua hii ni ile ya ushindi na pia hatua ya pili ya wokovu. Mwanadamu anatwaliwa na Mungu kupitia hukumu na kuadibu na neno; kwa kutumia neno kusafisha, hukumu na kufichua, uchafu wote, fikira, nia, na matumaini ya mtu mwenyewe katika moyo wa mwanadamu zinafuliwa. Ingawa mwanadamu amekombolewa na kusamehewa dhambi zake, inachukuliwa kuwa Mungu hakumbuki makosa ya mwanadamu na kutomtendea mwanadamu kulingana na makosa yake. Hata hivyo, mwanadamu anapoishi katika mwili na hajaachiliwa huru kutoka kwa dhambi, ataendelea tu kutenda dhambi, akiendelea kufunua tabia yake potovu ya kishetani. Haya ndiyo maisha ambayo mwanadamu anaishi, mzunguko usiokoma wa dhambi na msamaha. Wengi wa wanadamu wanatenda dhambi mchana kisha wanakiri jioni. Hivi, hata ingawa sadaka ya dhambi ni ya manufaa kwa binadamu milele, haitaweza kumwoko mwanadamu kutoka kwenye dhambi. Ni nusu tu ya kazi ya wokovu ndiyo imemalizika, kwani mwanadamu bado yuko na tabia potovu. Kwa mfano, wakati ambapo watu walijua kwamba walitoka kwa Moabu, walitoa maneno ya malalamiko, hawakutafuta tena uzima, na wakawa hasi kabisa. Je, hili halionyeshi kwamba bado hawawezi kutii kwa ukamilifu kutawaliwa na Mungu? Je, hii siyo tabia ya kishetani ya upotovu kabisa? Ulipokuwa hupitii kuadibu, mikono yako iliinuliwa juu zaidi ya wengine wote, hata ile ya Yesu. Na ulilia kwa sauti kubwa: “Kuwa mwana mpendwa wa Mungu! Kuwa mwandani wa Mungu! Ni heri tufe kuliko kumtii Shetani! Muasi Shetani wa zamani! Liasi joka kuu jekundu! Acha joka kuu jekundu lianguke kabisa kutoka mamlakani! Acha Mungu atufanye kamili!” Vilio vyako vilikuwa vikubwa zaidi ya wengine. Lakini kisha ukaja wakati wa kuadibu na, mara tena, tabia ya upotovu ya watu ilifichuliwa. Kisha, vilio vyao vikakoma, na hawakuwa tena na azimio. Huu ni upotovu wa mwanadamu; unaingia ndani zaidi kuliko dhambi, ulipandwa na Shetani na umekita mizizi ndani zaidi ya mwanadamu. Sio rahisi kwa mwanadamu kuzifahamu dhambi zake; mwanadamu hawezi kufahamu asili yake iliyokita mizizi. Ni kupitia tu katika hukumu na neno ndipo mabadiliko haya yatatokea. Hapo tu ndipo mwanadamu ataendelea kubadilika kutoka hatua hiyo kuendelea. Mwanadamu alipiga kelele hivyo wakati uliopita kwa sababu mwanadamu hakuwa na ufahamu

wa tabia yake potovu ya asili. Huo ndio uchafu ulio ndani ya mwanadamu. Kotekote katika kipindi kirefu hivyo cha hukumu na kuadibu, mwanadamu aliishi katika mazingira ya mvutano. Je, haya yote hayakutimizwa kupitia kwa neno? Wewe pia hukulia kwa sauti ya juu kabla ya majaribio ya watendaji huduma? Ingia katika ufalme! Wale wote ambao wanalikubali jina hili wataingia katika ufalme! Wote watashiriki Mungu! Wakati ambapo majaribio ya watendaji huduma yalikuja, hukulia tena. Mwanzoni, wote walilia, “Mungu! Popote Uniwekapo, nitatii kuongozwa na Wewe.” Baada ya kusoma maneno ya Mungu, “Nani atakuwa Paulo Wangu?” watu walisema, “Niko radhi!” Kisha wakayaona maneno, “Na kuhusu imani ya Ayubu?” Kwa hiyo akasema, “Niko radhi kuichukua imani ya Ayubu. Mungu, tafadhali nijaribu!” Majaribio ya watendaji huduma yalipokuja, walizirai mara moja na kusimama tena kwa nadra sana. Baada ya hilo, uchafu ndani ya moyo wa wao ulipungua polepole. Je, hili halikutimizwa kupitia kwa neno? Kwa hiyo, kile ambacho mmepitia wakati wa sasa ni matokeo ambayo hutimizwa kupitia kwa neno, hata makuu zaidi ya yale ambayo hutimizwa kupitia kwa Yesu kufanya ishara na maajabu. Utukufu wa Mungu na mamlaka ya Mungu Mwenyewe ambayo ninyi huona hayaonekani tu kupitia kwa usulubishaji, uponyaji wa magonjwa na ufukuzaji wa pepo, lakini zaidi kupitia kwa hukumu ya neno Lake. Hili hukuonyesha wewe kwamba sio tu ufanyaji wa ishara, uponyaji wa magonjwa na ufukuzaji wa pepo ndiyo mamlaka na nguvu za Mungu, bali kwamba hukumu ya neno la Mungu inaweza kuwakilisha vyema zaidi mamlaka ya Mungu na kufichua uweza Wake.

Kile ambacho mwanadamu amepata sasa—kimo cha mwanadamu leo, maarifa yao, upendo, uaminifu, utiifu, na pia kuona kwao—ni matokeo yanayopatikana kupitia hukumu ya neno. Kwamba unaweza kuwa na uaminifu na kubaki umesimama mpaka siku hii ipatikane kwa kupita neno. Hivi sasa mwanadamu anaona kuwa kazi ya Mungu kupata mwili ni ya ajabu kweli. Kuna mengi ambayo hayawezi kupatikana na mwanadamu, na kwamba ni mafumbo na maajabu. Kwa hivyo, wengi wamejiwasilisha. Wengine hawajawahi kujiwasilisha kwa mwanadamu yeyote kutoka siku za kuzaliwa kwao, ilhali wanapoyaona maneno ya Mungu siku hii, wanajiwasilisha kikamilifu bila kujua wamefanya vile, na hawajaribu kuchunguza au kusema chochote kingine. Binadamu wameanguka chini ya neno na wamesujudu chini ya hukumu ya neno. Kama Roho wa Mungu angemwongelesha wanadamu moja kwa moja, wote wangejiwasilisha kwa sauti hiyo, na kuanguka chini bila maneno ya ufunuo, vile Paulo alivyoanguka chini kukiwa na nuru alipokuwa akisafiri kwenda Damaski. Mungu angeendelea kufanya kazi kwa njia hii, mwanadamu hangeweza kutambua upotovu wake kupitia kwa hukumu ya neno na kupata wokovu. Ni kwa kupata mwili pekee ndiyo Mungu ataweza kuwasilisha maneno Yake Mwenyewe kwa masikio ya wale wote ambao wana masikio waweze kuyasikia maneno Yake na kupokea kazi Yake ya hukumu kupitia kwa neno. Hayo tu ndio matokeo yanayopokewa na neno Lake, badala ya kutokea kwa Roho ikimtisha mwanadamu kuwasilisha. Ni kupitia tu kwa kazi ya vitendo na ya

ajabu ndio tabia ya mwanadamu, iliyofichika ndani zaidi kwa enzi nyingi, ifichuliwe kabisa ili mwanadamu aitambue na kuibadilisha. Hili ndiyo kazi ya vitendo ya Mungu mwenye mwili; Ananena na kutekeleza hukumu kwa njia ya vitendo ili kupata matokeo ya hukumu juu ya mwanadamu kupitia kwa neno. Haya ndiyo mamlaka ya Mungu mwenye mwili na umuhimu wa Mungu kupata mwili. Inafanyika kuonyesha mamlaka ya Mungu mwenye mwili, matokeo yanayopatikana na kazi ya neno, na kwamba Roho Amekuja kwa mwili; Anaonyesha mamlaka Yake kupitia hukumu juu ya mwanadamu kwa neno. Ingawa mwili Wake ni hali ya nje ya mwanadamu wa kawaida, ni matokeo ambayo neno Lake linapokea ndiyo yanamwonyesha mwanadamu kuwa Amejaa mamlaka, kwama ni Mungu Mwenyewe na kwamba maneno Yake ni maonyesho ya Mungu Mwenyewe. Hii inaonyesha wanadamu wote kuwa Yeye ni Mungu Mwenyewe, Mungu Mwenyewe Aliyekuwa mwili, kwamba hapaswi kukosewa na yeyote na kwamba hakuna anayeweza kuepuka hukumu Yake kupitia kwa neno, na hakuna nguvu ya giza inayoweza kutamalaki juu ya mamlaka Yake. Mwanadamu anamtii Yeye kabisa kwa sababu Yeye ni Neno aliyepata mwili, kwa sababu ya mamlaka Yake, na kwa sababu ya hukumu Yake kwa neno. Kazi iliyoletwa na mwili Wake uliokuwa mwili ni mamlaka ambayo Anamiliki. Anakuwa mwili kwani mwili pia unaweza kuwa na mamlaka, na Anaweza kutekeleza kazi kati ya wanadamu katika hali ya njia halisi, inayoonekana na kuguswa na mwanadamu. Kazi kama hii ni ya ukweli kuliko kazi ingine yoyote ifanywayo moja kwa moja na Roho wa Mungu Aliye na mamlaka yote, na matokeo Yake ni dhahiri pia. Hii ni kwa sababu mwili wa Mungu unaweza kuongea na kufanya kazi kwa njia halisi; hali ya nje ya mwili Wake haina mamlaka yoyote na inaweza kukaribiwa na mwanadamu. Dutu Yake inabeba mamlaka, lakini mamlaka Yake hayaonekani kwa yeyote. Anaponena na kufanya kazi, mwanadamu hana uwezo wa kutambua uwepo wa mamlaka Yake; hili ni nzuri kwa kazi Yake hata zaidi. Hii kazi yote inaweza kupata matokeo. Ingawa hakuna mwanadamu anayefahamu kuwa Anayo mamlaka ama kuona kuwa Hastahili kukosewa ama kuona hasira Yake, kupitia mamlaka Yake yaliyofichika na hasira na hotuba ya uma, Anapata matokeo yaliyotarajiwa ya neno Lake. Kwa maneno mengine, kupitia kwa tani ya sauti Yake, ukali wa hotuba Yake, na hekima ya maneno Yake, mwanadamu anashawishika kabisa. Kwa njia hii, mwanadamu anawasilisha kwa neno la Mungu mwenye mwili wa Mungu, ambaye anaonekana kutokuwa na mamlaka, hivyo kufikia lengo la Mungu la wokovu kwa mwanadamu. Huu ndio umuhimu mwingine wa kuingia Kwake katika mwili: kuongea na ukweli zaidi na kukubali ukweli wa neno Lake kuwa na athari juu ya mwanadamu ili kushuhudia nguvu ya neno la Mungu. Kwa hivyo kazi hii isingefanywa kupitia kupata mwili, isingekuwa na matokeo hata kidogo na isingeweza kuokoa watenda dhambi kikamilifu. Mungu Asipokuwa mwili, Atabaki kama Roho bila kuonekana au kuguswa na mwanadamu. Mwanadamu ni kiumbe wa mwili, na mwanadamu na Mungu ni wa dunia mbili tofauti na ina asili tofauti tofauti. Roho wa Mungu hana uwiano na mwili wa mwanadamu, na hakuna uhusiano

unaoweza kuwepo kati yao; pia, mwanadamu hawezi kuwa roho. Hivyo, Roho wa Mungu lazima ageuke mmoja wa viumbe na kufanya kazi yake ya asili. Mungu anaweza kujipandisha mahali pa juu zaidi na pia aweze kunyenyekea na kuwa mwanadamu aliyeumbwa, kufanya kazi na kuishi kati ya wanadamu, lakini mwanadamu hawezi kupanda juu na kuwa roho na pia kuteremka chini. Kwa hivyo, Mungu lazima awe mwili ili ateleze kazi Yake. Kama ilivyokuwa wakati wa kuingia katika mwili mara ya kwanza, mwili wa Mungu mwenye mwili pekee ndio unaoweza kumkomboa mwanadamu kupitia kusulubiwa, ilhali hakuna uwezo wa Roho wa Mungu kusulubiwa kama sadaka ya dhambi kwa mwanadamu. Mungu Angekuwa mwili moja kwa moja ili kuwa sadaka ya dhambi kwa mwanadamu, lakini mwanadamu hangepanda mbinguni moja kwa moja kuchukua sadaka ambayo Mungu alikuwa amewaandalia. Hivyo, lazima Mungu asafiri kwenda na kurudi kati ya mbingu na nchi, badala ya kumwacha mwanadamu apande mbinguni kuchukua wokovu huu, kwani mwanadamu alikuwa ameanguka na, aidha, hangeweza kabisa kupaa mbinguni, ama hata kupata sadaka ya dhambi. Kwa hivyo, ilikuwa lazima kwa Yesu kuja kati ya wanadamu na binafsi kufanya kazi ambayo mwanadamu hangeweza kukamilisha. Kila wakati ambapo Mungu aligeuka kuwa mwili, ilikuwa lazima kabisa Afanye hivyo. Iwapo hatua yoyote ingetekelezwa moja kwa moja na Roho wa Mungu, Hangevumilia ukosefu wa hadhi unaoambatana na kupata mwili.

Katika hatua hii ya mwisho ya kazi, matokeo yanapatikana kupitia kwa neno. Kupitia kwa neno, mwanadamu anaelewa mafumbo mengi na kazi ya Mungu katika vizazi vilivyopita; kupitia kwa neno, mwanadamu anapewa nuru na Roho Mtakatifu; kupitia kwa neno, mwanadamu anapata kuelewa mafumbo ambayo hayajawahi kuelezwa na vizazi vilivyopita, na pia kazi za manabii na, mitume wa enzi zilizopita, na kanuni ambazo walitumia kufanya kazi; kupitia kwa neno, mwanadamu anatambua tabia ya Mungu Mwenyewe, na pia uasi na pingamizi ya mwanadamu, na anakuja kujua dutu yake mwenyewe. Kupitia kwa hatua hizi za kazi na maneno yote yaliyonenwa, mwanadamu anatambua kazi ya Roho Mtakatifu, kazi ya mwili wa Mungu, na zaidi ya hayo, tabia Yake yote. Maarifa yako ya kazi ya usimamizi wa Mungu wa kupita miaka elfu sita ulitwaliwa kupitia kwa neno. Je, maarifa yako hayakuwa ya fikira zako za awali na mafanikio kwa kuyaweka kando pia yalipatikana kupitia neno? Katika hatua ya awali, Yesu Alifanya ishara na maajabu, lakini sio hivyo katika hatua hii. Je si kuelewa kwako kwa nini Mungu hafanyi ishara na maajabu pia kulipatikana kupitia neno? Kwa hivyo, maneno yanenwayo katika hatua hii, yanashinda kazi iliyofanywa na mitume na manabii wa vizazi vilivyopita. Hata unabii uliotabiriwa na manabii haungeweza kupata matokeo haya. Manabii waliongelea unabii pekee, ya kile kitakachotendeka hapo baadaye, lakini sio kazi ambayo Mungu angefanya katika wakati huo. Hawakuongea kuwaongoza wanadamu katika maisha yao, kuwapa wanadamu ukweli ama kumfichulia mwanadamu mafumbo, ama hata kutawaza maisha. Kwa

maneno yaliyonenwa katika hatua hii, kuna unabii na ukweli, lakini hasa yanafanya kazi ya kutawaza maisha juu ya mwanadamu. Maneno ya wakati huu sio kama unabii wa manabii. Hii ni hatua ya kazi isiyo ya unabii ila ya maisha ya mwanadamu, kubadili tabia ya maisha ya mwanadamu. Hatua ya kwanza ilikuwa kazi ya Yehova kutengeneza njia ya mwanadamu kuabudu Mungu duniani. Ilikuwa kazi ya kuanzisha kutafuta chanzo cha kazi duniani. Wakati huo, Yehova aliwafunza Waisraeli kuiheshimu Sabato, wawaheshimu wazazi wao na kuishi kwa amani na wengine. Hii ilikuwa kwa sababu watu wa wakati huo hawakuwa ni nini kilichukuliwa kuwa mwanadamu, wala hawakuelewa walivyopaswa kuishi duniani. Ilikuwa lazima Kwake katika hatua ya kwanza ya kazi kuwaongoza wanadamu katika maisha yao. Yote yale Yehova aliwazungumzia hayakuwa yamewahi kujulikana kwa binadamu ama kuwa katika umiliki wao. Wakati huo, Mungu aliwainua manabii wengi kunena unabii, yote kutengenezwa chini ya uongozi wa Yehova. Hii ilikuwa sehemu moja ya kazi ya Mungu. Katika hatua ya kwanza, Mungu hakuwa mwili, hivyo Alizungumza na makabila yote na mataifa kupitia kwa manabii. Yesu alipofanya kazi Yake katika huo wakati, Hakuzungumza sana kama wakati huu wa leo. Kazi hii ya neno katika siku za mwisho haijafanyika katika enzi na vizazi vilivyopita. Ingawa Isaya, Danieli na Yohana walitabiri utabiri mwingi, unabii huo ulikuwa tofauti kabisa na maneno yazungumzwayo sasa. Walichoongelea ulikuwa unabii pekee, lakini maneno ya sasa sio unabii. Iwapo Ningebadilisha Ninayoongea sasa yawe unabii, je mngeweza kuyaelewa? Iwapo yale niliyozungumzia yangehusu mambo baada ya Mimi kuondoka, ungewezaje basi kupata kuelewa? Kazi ya neno haikuwahi kufanyika wakati wa Yesu ama Enzi ya Sheria. Labda wengine wanaweza kusema, “Je Yehova hakuzungumza maneno pia katika wakati wa kazi Yake? Juu yaa kuponya magonjwa, kukemea mapepo na kufanya ishara na maajabu, je Yesu hakuzungumza katika wakati huo?” Kuna tofauti katika vile maneno yananenwa. Ni nini ndiyo ilikuwa dutu ya maneno yaliyonenwa na Yehova? Alikuwa tu Akiwaongoza wanadamu katika maisha yao duniani, ambayo hayakuwa yanahusiana na mambo ya kiroho katika maisha. Ni kwa nini inasemekana kuwa maneno ya Yehova yalitangazwa katika sehemu zote? Neno “kufundisha” linamaanisha kuwaambia waziwazi na kuamrisha moja kwa moja. Hakupa mwanadamu maisha; ila, Alimchukua mwanadamu kwa mkono na kumfunza jinsi ya kumheshimu sana. Hakukuwa na mafumbo. Kazi ya Yehova katika Israeli haikuwa kushughulika na ama kumwadhibu mwanadamu ama kutoa hukumu na kuadibu, ilikuwa kuongoza. Yehova alimwambia Musa awaeleze watu Wake wakusanye mana jangwani. Kila asubuhi kabla ya jua kuchomoza, walikuwa wakusanye mana, iliyotosha tu kuliwa siku hiyo. Mana haingewekwa hadi siku inayofuata, kwani ingeoza. Hakuwakaripia wanadamu au kufichua asili zao, wa Hakufichua mawazo yao na fikira. Hakuwabadilisha watu ila tu aliwaongoza katika maisha yao. Katika wakati huo, watu walikuwa kama watoto; mwanadamu hakuelewa chochote na angefanya hatua za kuelekezwa, na hivyo, Yehova aliamuru tu sheria kuongoza watu.

Ili kueneza injili, ili walewote wanaotafuta kwa moyo wa kweli wapate maarifa ya kazi inayofanywa katika siku hii na kushawishika kabisa, lazima uielewe hadithi ya ndani, dutu na umuhimu wa kazi iliyofanywa katika kila hatua. Kwa kusikia ushirika wako, wataelewa kazi ya Yehova na kazi ya Yesu na, zaidi ya hayo, kazi yote ya Mungu wa leo, na vilevile uhusiano na tofauti kati ya hatua hizo tatu za kazi, ili kwamba, baada ya wao kusikiza, wataona kuwa hakuna hatua yoyote kati ya hizo tatu inahitilafiana na nyingine. Kwa hakika, yote yamefanywa na Roho mmoja. Ingawa Wanafanya kazi katika enzi tofauti, maudhui ya kazi Wanayotekeleza ni tofauti, na maneno Wanayozungumza ni tofauti, lakini kanuni ambazo Wanafanya kazi nazo ni sawa. Haya ndiyo maono makuu zaidi ambayo watu wote wanaomfuata Mungu wanapaswa kuelewa.

Kupata Mwili Mara Mbili Kunakamilisha Umuhimu wa Kupata Mwili

Kila hatua ya kazi iliyofanywa na Mungu ina umuhimu wake mkubwa. Yesu alipokuja zamani, Alikuwa mwanaume, lakini Mungu anapokuja wakati huu Yeye ni mwanamke. Kutokana na hili, unaweza kuona kwamba Mungu aliwaumba mwanaume na mwanamke kwa ajili ya kazi Yake na Kwake hakuna tofauti ya jinsia. Roho Wake anapowasili, Anaweza kuchukua mwili wowote kwa matakwa Yake na mwili huo unaweza kumwakilisha Yeye. Uwe wa kiume au kike, unaweza kumwakilisha Mungu alimradi tu ni mwili Wake wa nyama. Kama Yesu angeonekana kama kike alipokuja, kwa maneno mengine, iwapo mtoto wa kike, sio wa kiume, angezaliwa kwa njia ya Roho Mtakatifu, hatua hiyo ya kazi ingekuwa imekamilika pia. Kama hali ingekuwa hivyo, basi hatua ya leo ya kazi ingelazimika kukamilishwa badala yake na mwanaume, lakini kazi ingekamilika pia. Kazi inayofanywa katika hatua hizi zote ni muhimu kwa kiwango sawa; hakuna hatua yoyote ya kazi inayojirudia au kupingana na nyingine. Wakati huo, Yesu alipokuwa akifanya kazi Yake aliitwa Mwana wa pekee, na “Mwana” inaashiria jinsia ya kiume. Basi kwa nini Mwana wa pekee halikutajwa katika hatua hii? Hii ni kwa sababu mahitaji ya kazi yamelazimisha badiliko la jinsia ambayo ni tofauti na ile ya Yesu. Kwa Mungu hakuna tofauti ya jinsia. Kazi Yake inafanywa kama Anavyotaka na katika kufanya kazi Yake hazuiliwi na kitu chochote kile, lakini hasa yupo huru. Hata hivyo, kila hatua ya kazi ina umuhimu wake mkubwa. Mungu alipata mwili mara mbili, na ni dhahiri kwamba kupata mwili Kwake katika siku za mwisho ni mara ya mwisho. Amekuja kufichua matendo Yake yote. Ikiwa katika hatua hii Hakupata mwili ili Yeye binafsi afanye kazi kwa ajili ya mwanadamu kushuhudia, mwanadamu milele angeshikilia fikra kwamba Mungu ni wa kuime tu, na si wa kike. Kabla ya hili, wanadamu wote waliamini kwamba Mungu angeweza kuwa tu mwanaume na kwamba mwanamke hawezi kuitwa Mungu, maana wanadamu wote walimchukulia mwanamume kuwa na mamlaka juu ya mwanamke. Waliamini kwamba hakuna mwanamke

anayeweza kuchukua mamlaka, bali ni mwanamume tu. Aidha hata walisema kwamba mwanamume alikuwa ni mkuu wa mwanamke na kwamba mwanamke anapaswa kumtii mwanaume na asimshinde. Iliposemwa hapo nyuma kwamba mwanamume alikuwa mkuu wa mwanamke, ilielekezwa kwa Adamu na Hawa ambao walikuwa wamedanganywa na yule nyoka, na wala sio kwa mwanamume na mwanamke kama walivyoumbwa na Yehova hapo mwanzo. Bila shaka, mwanamke anapaswa kumtii na kumpenda mume wake, na mume anapaswa kujifunza kuilisha na kuiruzuku familia yake. Hizi ni sheria na kanuni zilizowekwa na Yehova ambazo kwazo wanadamu wanapaswa kuzifuata katika maisha yao ya hapa duniani. Yehova alimwambia mwanamke “Ashiki yako itakuwa kwa mume wako, na atatawala juu yako.” Alisema hivyo tu ili kwamba wanadamu (yaani, mwanamume na mwanamke) waweze kuishi maisha ya kawaida chini ya utawala wa Yehova, na tu ili kwamba maisha ya wanadamu yaweze kuwa na mfumo na yasipoteze mwelekeo. Kwa hivyo, Yehova alitengeneza kanuni zinazofaa ya namna ambavyo mwanamume na mwanamke wanavyopaswa kutenda, lakini hili lilihusu tu viumbe wote wanaoishi duniani na halikuhusiana na mwili wa Mungu wa nyama. Inawezekanaje Mungu awe sawa na viumbe Wake? Maneno Yake yalielekezwa tu kwa wanadamu wa viumbe Wake; Alianzishia mwanamume na mwanamke kanuni ili wanadamu waweze kuishi maisha ya kawaida. Hapo mwanzo, Yehova alipoumba wanadamu, Aliwaumba wanadamu wa aina mbili, mwanamume na mwanamke; na kwa hiyo, kuna mgawanyo wa kike na kiume katika miili Yake. Hakuamua juu ya kazi Yake kulingana na maneno aliyozungumza kwa Adamu na Hawa. Mara mbili Alipopata mwili kuliamuliwa kwa kuzingatia kabisa mawazo Yake alipowaumba wanadamu kwa mara ya kwanza, yaani, Alikamilisha kazi ya kupata Kwake mwili mara mbili, kwa msingi wa mwanamke na mwanamume kabla ya wao kupotoshwa. Ikiwa wanadamu wangechukua maneno yaliyozungumzwa na Yehova kwa Adamu na Hawa, ambao walikuwa wamedanganywa na yule nyoka, na kuyatumia katika kazi ya mwili wa Mungu, je, si Yesu pia angepaswa kumpenda mke Wake kama Alivyotakiwa? Je, kwa njia hii, Mungu bado ni Mungu? Na ikiwa ni hivyo, je, bado Angeweza kukamilisha kazi Yake? Ikiwa ni vibaya kwa mwili wa Mungu kuwa mwanamke, je, basi lisingekuwa kosa kubwa sana pia kwa Mungu kumuumba mwanamke? Ikiwa mwanadamu bado anaamini kwamba Mungu kupata mwili kama mwanamke ni vibaya, je, basi Yesu, ambaye hakuoa na hivyo hakuweza kumpenda mke Wake, angekuwa na makosa kama kupata mwili wa sasa? Kwa kuwa unatumia maneno yaliyozungumzwa na Yehova kwa Hawa ili kupima ukweli wa Mungu kupata mwili leo, basi unapaswa kutumia maneno ya Yehova kwa Adamu kumhukumu Bwana Yesu ambaye alipata mwili katika Enzi ya Neema. Je, hawa wawili sio sawa? Kwa kuwa unampima Bwana Yesu kulingana na mwanamume ambaye hakuwa amedanganywa na yule nyoka, basi hupaswi kuhukumu ukweli wa kupata mwili leo hii kulingana na mwanamke ambaye alikuwa amedanganywa na yule nyoka. Hili si haki! Ikiwa umefanya hukumu ya namna hiyo, inathibitisha kukosa urazini kwako. Yehova alipopata mwili

mara mbili, jinsia ya mwili Wake ilikuwa inahusiana na mwanamume na mwanamke ambaye hakuwa amedanganywa na yule nyoka; Alipata mwili mara mbili kulingana na mwanamume na mwanamke ambaye hakuwa amedanganywa na yule nyoka. Usifikiri kwamba uanaume wa Yesu ulikuwa sawa na uanaume wa Adamu ambaye alidanganywa na yule nyoka. Hahusiani naye kabisa, na ni wanaume wawili wa asili tofauti. Hakika haiwezi kuwa kwamba uanaume wa Yesu unathibitisha Yeye ni mkuu wa wanawake wote lakini sio mkuu wa wanaume wote? Je, Yeye si Mfalme wa Wayahudi wote (ikiwa ni pamoja na wanaume na wanawake)? Yeye ni Mungu Mwenyewe, sio tu mkuu wa mwanamke bali mkuu wa mwanamume pia. Yeye ni Bwana wa viumbe vyote, na mkuu wa viumbe vyote. Unawezaje kuamua uanaume wa Yesu kuwa ishara ya mkuu wa mwanamke? Huku si kukufuru? Yesu ni mwanamume ambaye hajapotoshwa. Yeye ni Mungu; Yeye ni Kristo; Yeye ni Bwana. Anawezaje kuwa mwanamume kama Adamu ambaye alipotoshwa? Yesu ni mwili uliovaliwa na Roho wa Mungu aliye mtakatifu sana. Unawezaje kusema kuwa Yeye ni Mungu aliye na uanaume wa Adamu? Kama ni hivyo, kazi yote ya Mungu haingekuwa si sahihi? Je, Yehova angeweza kuuweka ndani ya Yesu uanaume wa Adamu ambaye alidanganywa na yule nyoka? Je, si kupata mwili kwa wakati huu ni tukio jingine la kazi ya Mungu mwenye mwili ambaye ni tofauti kijinsia na Yesu lakini aliye kama Yeye katika asili? Bado unathubutu kusema kwamba Mungu mwenye mwili hawezi kuwa mwanamke kwa kuwa mwanamke ndiye aliyedanganywa kwanza na yule nyoka? Bado unathubutu kusema kwamba, kwa kuwa mwanamke ndiye mwenye najisi sana na ni chanzo cha upotovu wa wanadamu, Mungu hawezi kabisa kupata mwili kama mwanamke? Bado unathubutu kuendelea kusema kwamba “mwanamke siku zote atamtii mwanamume na hawezi kamwe kudhihirisha au kumwakilisha Mungu moja kwa moja”? Hukuelewa hapo nyuma; lakini sasa bado unaweza kuendelea kukufuru kazi ya Mungu, hususan mwili wa nyama wa Mungu? Kama huwezi kuona hili kwa uwazi kabisa, ni vizuri zaidi ukawa makini na ulimi wako, la sivyo upumbavu na ujinga wako ufichuliwe na ubaya wako uwekwe wazi. Usidhani kwamba unaelewa kila kitu. Nakueleza kwamba yote uliyokwishayaona na kuyapitia hayakutoshelezi wewe kuelewa hata sehemu ndogo kabisa ya mpango Wangu wa usimamizi. Hivyo kwa nini basi unakuwa mwenye kiburi sana? Talanta ndogo hiyo uliyonayo na maarifa kidogo hayo uliyonayo hayatoshelezi kutumika na Yesu hata katika sekunde moja ya kazi Yake! Je, una uzoefu kiasi gani hasa? Yale uliyoyaona na yote uliyoyasikia katika maisha yako yote na yale uliyoyafikiria ni kidogo kuliko kazi Ninayoifanya kwa muda mfupi sana! Ni bora usichambue na kutafuta kosa. Haijalishi una kiburi kiasi gani, wewe bado ni kuimbe tu mdogo kuliko mchwa! Vyote vilivyomo katika tumbo lako ni vichache zaidi ya vile vilivyomo katika tumbo la mchwa! Usifikiri kwamba kwa kuwa tu umepata uzoefu na ukubwa kiasi, unaweza kuashiria kiburi na kuzungumza kwa maringo. Je, uzoefu wako na ukubwa wako sio matokeo ya maneno Niliyoyazungumza? Je, unaamini kwamba yalikuwa mbadala wa kufanya kwako kazi kwa bidii na kutokwa jasho? Siku hii,

unaona kuwa nimepata mwili, na kwa sababu ya hili pekee unajawa na dhana nyingi hizo, na kutoka kwalo unakuwa na fikira nyingi isiyohesabika. Ingekuwa kwa kupata mwili Kwangu, bila kujali talanta ulizo nazo ni za ajabu kiasi gani, usingekuwa na dhana hizi nyingi; si ni kutoka hapa ndipo fikira zako zinatoka hapa? Kama si kupata mwili kwa Yesu mara hiyo ya kwanza, je, hata ungejua kuhusu kupata mwili? Je, si kwa sababu ya maarifa yako kutoka kwa kupata mwili mara ya kwanza ndio una ufidhuli kuthubutu kuhukumu kupata mwili kwa mara ya pili? Kwa nini ukuchunguze badala ya kuwa mfuasi mtiifu? Wakati umeingia katika mkondo huu na kuja mbele ya Mungu mwenye mwili, je, Angekuruhusu kuchunguza hili? Ni sawa kwako kuchunguza historia ya familia yako, lakini ukijaribu kuchunguza “historia ya familia” ya Mungu, inawezekanaje Mungu wa leo akuruhusu kufanya uchunguzi kama huo? Je, wewe si kipofu? Je, hujiletei dharau kwako mwenyewe?

Ikiwa tu kazi ya Yesu ingefanywa bila kukamilishwa na kazi katika hatua hii ya siku za mwisho, basi mwanadamu milele angeshikilia fikira kwamba Yesu tu ndiye Mwana wa pekee wa Mungu, yaani, Mungu ana mwana mmoja tu, na kwamba yeyote anayekuja baada yake akiwa na jina jingine hawezi kuwa Mwana pekee wa Mungu, sembuse Mungu Mwenyewe. Mwanadamu ana fikira kwamba yeyote ambaye anajitoa sadaka kwa ajili ya dhambi au yule ambaye anachukua mamlaka kwa niaba ya Mungu na anayewakomboa wanadamu wote ni Mwana wa Mungu wa pekee. Kuna baadhi ambao wanaamini kwamba alimradi Yeye anayekuja ni mwanamume, Anaweza kuchukuliwa kuwa ni Mwana wa Mungu wa pekee na mwakilishi wa Mungu, na hata kuna wale wanaosema kwamba Yesu ni Mwana wa Yehova, Mwana Wake wa pekee. Je, hii kweli siyo tu fikira iliyopita kiasi ya mwanadamu? Ikiwa hatua hii ya kazi haingefanywa katika enzi ya mwisho, basi wanadamu wote wangekuwa gizani sana kumhusu Mungu. Ingekuwa ni hivyo, mwanamume angejidhania kuwa ni wa juu sana kuliko mwanamke, na wanawake hawangeweza kamwe kuinua vichwa vyao juu na hivyo, hakuna mwanamke angeweza kuokolewa. Watu siku zote wanaamini kwamba Mungu ni mwanamume, na aidha kwamba siku zote Amemchukia mwanamke na asingempa wokovu. Ingekuwa ni hivyo, isingekuwa ukweli kwamba wanawake wote walioumbwa na Yehova na pia ambao wamepotoshwa, wasingeweza kuwa na fursa ya kuokolewa? Je, basi isingekuwa bure kwa Yehova kumuumba mwanamke, yaani, kumuumba Hawa? Na je, mwanamke asingeangamia milele? Kwa hiyo, hatua ya kazi katika siku za mwisho inafanywa ili kuwaokoa wanadamu wote, sio mwanamke tu Ikiwa kunaye anayefikiria kwamba ikiwa Mungu angepata mwili kama kike, ingekuwa kwa ajili ya kumwokoa mwanamke pekee, basi mtu huyo bila shaka angekuwa mpumbavu!

Kazi inayofanywa kwa sasa imesukuma mbele kazi ya Enzi ya Neema; yaani, kazi katika mpango mzima wa usimamizi wa miaka elfu sita imesonga mbele. Ingawa Enzi ya Neema

imeisha, kazi ya Mungu imeendelea mbele. Kwa nini Ninasema mara kwa mara kwamba hatua hii ya kazi inajengwa juu ya Enzi ya Neema na Enzi ya Sheria? Hii ina maana kwamba kazi ya siku hii ni mwendelezo wa kazi iliyofanyika katika Enzi ya Neema na maendeleo ya kazi iliyofanyika katika Enzi ya Sheria. Hatua hizi tatu zinaingiliana kwa karibu na kuunganika moja kwa inayofuata kwa karibu. Kwa nini pia Ninasema kwamba hatua hii ya kazi inajengwa juu ya ile iliyofanywa na Yesu? Tuseme kwamba hatua hii haingejengwa juu ya kazi iliyofanywa na Yesu, ingebidi kusulubiwa kwingine kufanyike katika hatua hii, na kazi ya ukombozi ya hatua iliyopita ingelazimika kufanywa upya tena. Hii isingekuwa na maana yoyote. Kwa hiyo, sio kwamba kazi imekamilika kabisa, bali ni kwamba enzi imesonga mbele, na kiwango cha kazi kimewekwa juu kabisa kuliko kilivyokuwa kabla. Inaweza kusemwa kwamba hatua hii ya kazi imejengwa juu ya msingi wa Enzi ya Sheria na kwenye mwamba wa kazi ya Yesu. Kazi hii inajengwa hatua kwa hatua, na hatua hii sio mwanzo mpya. Ni muungano tu wa hatua tatu za kazi ndio unaweza kuchukuliwa kuwa mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita. Kazi ya hatua hii inafanywa kwa msingi wa kazi ya Enzi ya Neema. Ikiwa hatua hizi mbili za kazi hazikuhusiana, kwa nini basi kusulubiwa hakurudiwi katika hatua hii? Kwa nini Sibebi dhambi za mwanadamu, lakini badala yake Naja kumhukumu na kumwadibu mwanadamu moja kwa moja? Ikiwa kazi Yangu ya kumhukumu na kumwadibu mwanadamu na kuja Kwangu saa hii si kwa njia ya Roho Mtakatifu na hakukufuata kusulubiwa, basi Nisingekuwa na sifa zinazostahili kumhukumu na kumwadibu mwanadamu. Kazi katika hatua inajenga kabisa juu ya kazi katika hatua iliyotangulia. Hiyo ndiyo maana ni kazi kama hii tu ndiyo inaweza kumleta mwanadamu katika wokovu hatua kwa hatua. Yesu pamoja na Mimi tunatoka kwa Roho Mmoja. Ingawa miili Yetu haina uhusiano, Roho Zetu ni moja; ingawa kile Tunachofanya na kazi Tulizo nazo hazifanani, kwa asili Tunafanana; Miili Yetu ina maumbo tofauti, lakini hii ni kwa sababu ya mabadiliko ya enzi na mahitaji tofauti ya kazi Yetu; huduma Zetu hazifanani, hivyo kazi Tunayoileta na tabia Tunayoifichua kwa mwanadamu pia ni tofauti. Ndiyo maana kile ambacho mwanadamu anakiona na kukielewa leo hii si kama kile cha wakati uliopita; ni hivyo kwa sababu ya mabadiliko ya enzi. Ingawa jinsia na maumbo ya miili Yao ni tofauti, na kwamba hawakuzaliwa katika familia moja, sembuse katika kipindi kimoja, hata hivyo Roho Zao ni moja. Ingawa miili Yao haina uhusiano wa damu au kimwili kwa namna yoyote ile, haipingiki kwamba Wao ni Mungu kupata mwili katika vipindi viwili tofauti vya nyakati. Ni ukweli usiopingika kwamba Wao ni miili ya nyama ya Mungu, ingawa hawatoki katika ukoo mmoja na hawatumii lugha moja ya binadamu (mmoja alikuwa mwanamume aliyezungumza lugha ya Wayahudi na mwingine ni mwanamke anayezungumza Kichina pekee). Ni kwa sababu hizi ndiyo Wameishi katika nchi tofauti kufanya kazi ambayo inampasa kila mmoja kufanya, na katika nyakati tofauti vilevile. Licha ya ukweli kwamba Wao ni Roho moja, wakiwa na asili inayofanana, hakuna mfanano wa wazi kabisa kati ya ngozi za nje za miili Yao. Wanashiriki tu ubinadamu sawa,

lakini sura ya nje ya miili Yao na kuzaliwa Kwao hakufanani. Mambo haya hayana athari katika kazi Zao au maarifa aliyonayo mwanadamu juu Yao, maana, kimsingi, Wao ni Roho moja na hakuna anayeweza kuwatenganisha. Ingawa Hawana uhusiano wa damu, nafsi Zao zote zinaongoza Roho Zao, ambazo zinawapa kazi tofauti katika nyakati tofauti, na miili Yao kwa ukoo tofauti. Roho wa Yehova si baba wa Roho wa Yesu na Roho wa Yesu si mwana wa Roho wa Yehova: Ni Roho moja. Vile vile Kama vile Mungu mwenye mwili wa leo na Yesu. Ingawa Hawahusiani kwa damu, ni Wamoja; hii ni kwa sababu Roho Zao ni moja. Mungu anaweza kufanya kazi ya rehema na wema, vilevile na ile kazi ya hukumu ya haki na kumwadibu mwanadamu, na ile ya kuleta laana kwa mwanadamu; na hatimaye, Anaweza kufanya kazi ya kuuharibu ulimwengu na kuwaadhibu waovu. Je, hafanyi haya yote Mwenyewe? Je, hii si kudura ya Mungu? Aliweza kutangaza sheria kwa ajili ya mwanadamu na kumpa amri, na aliweza pia kuwaongoza Waisraeli wa awali katika kuishi maisha yao duniani na kuwaongoza kujenga hekalu na madhabahu, Akiwatawala Waisraeli wote. Kwa kutegemea mamlaka Yake, Aliishi pamoja na Waisraeli duniani kwa miaka elfu mbili. Waisraeli hawakuthubutu kumwasi; wote walimheshimu Yehova na walifuata amri Zake. Hii ilikuwa Kazi iliyofanywa kwa kutegemea mamlaka Yake na kudura Yake. Kisha, katika Enzi ya Neema, Yesu alikuja kuwakomboa wanadamu wote walioanguka (sio Waisraeli pekee). Alionyesha rehema na wema kwa mwanadamu. Yesu ambaye mwanadamu alimwona katika Enzi ya Neema Alikuwa amejazwa na wema na siku zote Alikuwa mwenye upendo kwa mwanadamu, maana Alikuwa amekuja kuwakomboa wanadamu kutoka dhambini. Aliweza kuwasamehe wanadamu dhambi zao hadi pale ambapo kusulubiwa Kwake kuliwakomboa wanadamu kutoka dhambini kabisa. Wakati huo, Mungu alionekana kwa mwanadamu kwa rehema na wema; yaani, Alijitoa sadaka kwa ajili ya mwanadamu na Alisulubiwa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu ili kwamba ziweze kusamehewa milele. Alikuwa mwenye rehema, mwenye huruma, mwenye upendo na mstahimilivu. Na wale wote waliomfuata Yesu katika Enzi ya Neema nao pia walitafuta kuwa wastahimilivu na wenye upendo katika mambo yote. Walistahimili mateso kwa muda mrefu, na hawakuwahi kulipiza kisasi hata walipopigwa, kulaaniwa au kupigwa mawe. Lakini haya hayawezi kuwa hivyo tena katika hatua ya mwisho. Vivyo hivyo, hata ingawa Roho Zao zilikuwa moja, kazi ya Yesu na Yehova hazikufanana kabisa. Kazi ya Yehova haikuwa kwa ajili ya kukamilisha enzi bali kuiongoza, kukaribisha maisha ya wanadamu duniani. Hata hivyo, kazi sasa ni kuwashinda wale walio katika mataifa yasiyo ya Wayahudi na ambao wamepotoshwa sana, sio tu watu wateule wa Mungu nchini China, bali ulimwengu mzima na wanadamu wote. Inaweza kuonekana kwako kwamba kazi hii inafanywa Uchina pekee, lakini kwa kweli imekwishaanza kusambaa katika nchi za ughaibuni. Ni kwa nini wageni mara kwa mara wanatafuta njia ya kweli? Hiyo ni kwa sababu Roho tayari amekwishaanza kazi, na maneno yanayonenwa sasa yanaelekezwa kwa watu ulimwenguni kote. Na hili, nusu ya kazi tayari

inafanywa. Kutoka kuumbwa kwa dunia hadi sasa, Roho wa Mungu ameendeleza hii kazi kubwa, na aidha Amefanya kazi tofauti katika enzi tofauti, na katika mataifa tofauti. Watu wa kila enzi wanaona tabia Yake tofauti, ambayo kwa asili inafichuliwa kupitia kazi tofauti Anazozifanya. Yeye ni Mungu, aliye mwingi wa rehema na wema; Yeye ni sadaka ya dhambi kwa ajili ya mwanadamu na mchungaji wa mwanadamu; lakini pia Yeye ni hukumu, kuadibu, na laana kwa mwanadamu. Angeweza kumwongoza mwanadamu kuishi duniani kwa miaka elfu mbili na pia Angeweza kuwaokoa wanadamu waliopotoka kutoka dhambi. Leo, pia Anaweza kuwashinda wanadamu ambao hawamjui na kuwafanya wawe chini ya miliki Yake, ili kwamba wote wajinyenyekeze kwake kikamilifu. Mwishowe, Atachoma yote ambayo si safi na ambayo ni dhalimu ndani ya wanadamu katika ulimwengu mzima, ili kuwaonyesha kwamba Yeye si Mungu wa Rehema, na upendo tu, si Mungu wa hekima, na maajabu tu, si Mungu mtakatifu tu, bali, hata zaidi ni Mungu anayemhukumu mwanadamu. Kwa waovu miongoni mwa wanadamu, Yeye ni mwenye kuchoma, kuhukumu na kuadhibu; kwa wale ambao wanapaswa kukamilishwa, Yeye ni mateso, usafishaji, na majaribu, na vilevile faraja, ruzuku, utoaji wa maneno, kushughulika na kupogoa. Na kwa wale ambao wanaondolewa, Yeye ni adhabu na vilevile malipo. Niambie, je, Mungu si mwenye enzi? Anaweza kufanya kazi yoyote na yote, sio tu kusulubiwa kama ulivyokuwa ukifikiri. Unamfikiria Mungu kuwa ni wa chini sana! Je, unaamini kwamba chote Anachoweza kufanya ni kukomboa wanadamu wote kupitia kusulubiwa kwako pekee? Na baada ya hilo, utamfuata mbinguni kula tunda kutoka mti wa uzima na kunywa kutoka mto wa uzima? ... Je, inaweza kuwa rahisi hivyo? Niambie, umekamilisha nini? Je, una uzima wa Yesu? Ni kweli ulikombolewa naye, lakini kusulubiwa kulikuwa ni kazi ya Yesu Mwenyewe. Ni wajibu gani umeukamilisha kama mwanadamu? Una uchaji Mungu wa nje pekee lakini huielewi njia Yake. Hivyo ndivyo unavyomdhihirisha? Ikiwa hujapata maisha ya Mungu au kuona tabia Yake yote ya haki, basi huwezi kudai kuwa mtu aliye na uzima, na hustahili kupitia katika lango la ufalme wa mbinguni.

Mungu si Roho pekee, Anaweza pia kuwa mwili. Aidha, Yeye ni mwili wa utukufu. Yesu, ingawa hamjamwona, alishuhudiwa na Waisraeli, yaani, Wayahudi wa wakati huo. Mwanzoni alikuwa mwili wa nyama, lakini baada ya kusulubiwa, Aligeuka mwili wa utukufu. Yeye ni Roho anayezunguka mambo yote na Anaweza kufanya kazi katika kila mahali. Anaweza kuwa Yehova, au Yesu au Masihi; hatimaye, Anaweza pia kuwa Mwenyezi Mungu. Yeye ni haki, hukumu, na kuadibu; Yeye ni laana na ghadhabu, lakini pia Yeye ni rehema na wema. Kazi zote ambazo Amezifanya zinaweza kumwakilisha. Unasema Yeye ni Mungu ni wa aina gani? Huwezi kuelezea kabisa. Iwapo huwezi kweli kueleza, hufai kufanya mahitimisho kumhusu Mungu. Usihitimishe kwamba Mungu milele ni Mungu wa rehema na wema, kwa sababu tu Yeye alifanya kazi ya ukombozi katika hatua moja. Je, unaweza kuwa na uhakika kwamba Yeye ni

Mungu wa rehema na upendo pekee? Ikiwa Yeye ni Mungu tu wa rehema na mwenye upendo, kwa nini Ataikomesha enzi katika siku za mwisho? Kutokana na fikira na mawazo ya watu Mungu anastahili kuwa mwenye rehema na upendo hadi katika enzi ya mwisho, ili kwamba kila mmoja wa wanadamu aweze kuokolewa. Lakini kwa nini, katika enzi za mwisho, ndipo Atatuma chini majanga makubwa kama vile mitetemeko ya ardhi, tauni na njaa ili kuwaangamiza wanadamu waovu, wanaomchukulia Mungu kama adui? Kwa nini anamruhusu mwanadamu kuteseka majanga haya? Hakuna yeyote kati wenu anayethubutu kusema Yeye ni Mungu wa aina gani, na hakuna anayeweza kuelezea. Je, unaweza kuwa na uhakika kwamba Yeye ni Roho? Je, unathubutu kusema kuwa Yeye ni mwili wa Yesu pekee? Na unathubutu kusema kuwa Yeye ni Mungu ambaye milele atasulubiwa kwa ajili ya mwanadamu?

Je, Utatu Upo?

Baada ya ukweli wa Yesu aliyepata mwili kutokea, mwanadamu aliamini hili: Si Baba pekee aliye mbinguni, bali pia Mwana, na hata Roho Mtakatifu. Hii ndiyo dhana ya kawaida aliyonayo mwanadamu, kwamba kuna Mungu wa aina hii mbinguni: Utatu ambao ni Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, wote katika nafsi moja. Wanadamu wote wana fikra hizi: Mungu ni Mungu mmoja, ila Anajumuisha sehemu tatu, kile ambacho wale wote waliofungwa kwa huzuni katika hizi dhana za kawaida wanachukulia kuwa kuna Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Ni sehemu hizo tatu pekee ambazo zimefanywa moja ambazo ni Mungu kamili. Bila Baba Mtakatifu, Mungu asingekuwa mkamilifu. Vivyo hivyo, wala Mungu asingekuwa mkamilifu bila Mwana au Roho Mtakatifu. Katika mawazo yao, wanaamini kuwa Baba au Mwana pekee havezi kuwa Mungu. Ni Baba, Mwana na Roho Mtakatifu tu kwa pamoja wanaoweza kuwa Mungu Mwenyewe. Sasa, waumini wote wa kidini, na hata kila mfuasi miongoni mwenu, anashikilia hii imani. Ilhali, ikiwa hii imani ni sahihi, hakuna anayeweza kuelezea, kwani daima mmechanganyikiwa kuhusu masuala ya Mungu Mwenyewe. Japo hizi ni fikra tu, hamjui kama ni sawa au mbaya, kwani mmeathiriwa vibaya na mawazo ya kidini. Mmeyakubali kwa kina haya mawazo ya kidini yaliyozoeleka, na hii sumu imezama kwa kina ndani yenu. Hivyo basi, hata kwa hili mmeanguka katika huu ushawishi wenye madhara, kwani Utatu haupo. Yaani, Utatu wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu haupo. Hizi zote ni fikra za kawaida za mwanadamu, na imani za uongo za mwanadamu. Kwa karne nyingi, mwanadamu ameamini katika huu Utatu, ambao umebuniwa na mawazo katika akili za mwanadamu, ukatengenezwa na mwanadamu, na ambao haujawahi kuonekana na mwanadamu. Kwa miaka mingi, kumekuwa na watu maarufu wa kiroho ambao wameeleza “maana ya kweli” ya Utatu, ila maelezo hayo ya Utatu kama nafsi tatu dhahiri yamekuwa si yakini na hayapo wazi na watu wote wamepumbazwa na “ujenzi” wa Mungu. Hakuna mtu maarufu yeyote aliyewahi kutoa maelezo kamili; maelezo mengi yanafaa katika masuala ya mjadala na katika maandishi, ila hakuna hata mtu mmoja ambaye ana ufahamu

kamili na wa wazi kuhusu maana ya Utatu. Hii ni kwa sababu huu Utatu huu mkuu ambao mwanadamu anashikilia moyoni kwa hakika haupo. Kwani hakuna aliyewahi kuiona sura ya Mungu au kubahatika kumtembelea katika makao Yake ili kuchunguza ni vitu gani vipo mahali ambapo Mungu anakaa, kubainisha wazi ni makumi mangapi ya maelfu, au mamia ya mamilioni ya vizazi yako katika “nyumba ya Mungu” au hata kuchunguza ni sehemu ngapi zimeuunga mwili wa asili wa Mungu Kinachofaa hasa kuchunguzwa ni: enzi ya Baba na Mwana, na vilevile Roho Mtakatifu; umbo la kila mmoja; hasa ni vipi Wanajitenganisha, na ni vipi Wanafanywa kuwa kitu kimoja. Kwa bahati mbaya, katika miaka hii yote, hakuna hata mtu mmoja ambaye ameweza kugundua ukweli wa haya mambo. Wote wanabuni tu, kwani hakuna hata mtu mmoja aliyewahi kwenda mbinguni kwa matembezi na kurejea na “ripoti ya uchunguzi” kwa wanadamu wote ili kuripoti kuhusu ukweli wa mambo kwa wale waumini wote wa kidini wenye bidii na wacha Mungu wanaojishughulisha sana na Utatu Mtakatifu. Bila shaka, mwanadamu hawezi kulaumiwa kwa kubuni na fikra hizo, maana kwa nini Yehova Baba hakuambatana na Yesu Mwana alipomuumba mwanadamu? Ingekuwa hapo mwanzoni kuwa wote waliitwa Yehova, ingekuwa bora zaidi. Ikiwa kuna wa kulaumiwa, wacha lawama iwe kwa kuteleza kwa muda kwa Yehova Mungu, ambaye hakuwaita Mwana na Roho Mtakatifu mbele Zake wakati wa uumbaji, ila badala yake Akafanya kazi Yake peke Yake. Ikiwa Wote Wangefanya kazi wakati mmoja, basi wasingekuwa kitu kimoja? Ikiwa, tangu mwanzo kabisa hadi mwisho, kungekuwa na jina moja tu Yehova pasipo jina la Yesu tangu Enzi ya Neema, au ikiwa Angeitwa bado Yehova, je, Mungu asingepushiwa na wanadamu taabu ya huu utangano? Kwa hakika, Yehova hawezi kulaumiwa kwa ajili ya haya yote; kama ni lawama, hebu na iwekwe kwa Roho Mtakatifu, ambaye kwa maelfu ya miaka Aliendelea na kazi yake kwa jina la Yehova, la Yesu, na hata la Roho Mtakatifu, Akiwachanganya na kuwakanganya wanadamu kiasi kwamba wanadamu wakashindwa kufahamu Mungu ni nani hasa. Iwapo Roho Mtakatifu angefanya kazi bila umbo au sura, aidha, bila jina kama vile Yesu, na mwanadamu asingemgusa wala kumuona, ila kusikia tu ngurumo za radi, basi si kazi hiyo ingekuwa ya manufaa zaidi kwa mwanadamu? Hivyo nini kinaweza kufanywa sasa? Fikra za mwanadamu zimerundikana juu kama mlima na kuenea kama bahari, kiasi kwamba Mungu wa sasa hawezi kuzistahimili kamwe na hajui la kufanya. Hapo nyuma wakati kulikuwa tu na Yehova, Yesu, na Roho Mtakatifu katikati ya hao wawili, mwanadamu tayari alikuwa amechanganyikiwa na jinsi ya kuvumilia, na sasa kuna ongezeko la mwenye Uweza, ambaye hata anasemekana kuwa sehemu ya Mungu. Ni nani anajua Yeye ni nani na Ameingiliana au kujificha kwa nani katika Utatu Mtakatifu kwa miaka mingapi? Mwanadamu anawezaje kulistahimili hili? Utatu Mtakatifu pekee ulitosha kumchukua mwanadamu milele kuueleza, lakini sasa kuna “Mungu mmoja katika nafsi nne.” Hili linaweza kuelezwa vipi? Unaweza kulieleza? Ndugu! Mameaminije katika Mungu huyu mpaka leo? Ninawavulia kofia. Utatu uliweza kuvumilika; mliwezaje kuendelea kuwa na imani isiyotikisika

namna hiyo katika huyu Mungu mmoja katika nafsi nne? Mmehimizwa muondoke na bado mnakataa. Ajabu iliyoje! Nyinyi ni watu wa ajabu! Mtu kweli anaweza kuendelea kuamini Mungu wanne na asiwaelewe; hamuoni kuwa huu ni muujiza? Sikujua kwamba mlikuwa na uwezo wa kutenda muujiza mkubwa kiasi hiki! Hebu Niwaambie hilo, kwa hakika, Mungu wa Utatu hayupo popote katika dunia hii. Mungu hana Baba wala Mwana, na sembuse Baba na Mwana hutumia kwa pamoja Roho Mtakatifu kama chombo. Huu wote ni uongo mkubwa zaidi na haupo kabisa katika dunia hii! Hata hivyo uongo huu una asili yake na haukosi msingi kabisa, kwani akili zenu si punguani, na mawazo yenu hayakosi mantiki. Badala yake, ziko sawa na yenye ubunifu kwa kiasi kikubwa, kwamba haziwezi kuzuiwa hata na Shetani yeyote. La kusikitisha ni kwamba mawazo haya ni uongo mtupu na hayapo kabisa! Hamjaona ukweli halisi haswa; mnabuni na kujiundia dhana, na kuzitengeneza kuwa hadithi ili kuteka imani ya wengine kwa uongo na kupata mamlaka miongoni mwa wanadamu wapumbavu wasio na busara, ili kwamba waamini katika “mafundisho yenu ya kitaaluma” makuu na mashuhuri. Je, huu ni ukweli? Je, hii ndiyo njia ya uzima ambayo wanadamu wanafaa kupokea? Huu ni upuuzi! Hakuna hata neno moja linafaa! Katika miaka hii yote, nyinyi mmegawanya Mungu namna hii, na kuendelea kugawanywa zaidi katika kila kizazi kiasi kwamba Mungu mmoja amegawanywa kuwa Mungu watatu. Na sasa haiwezekani kabisa kwa mwanadamu kumuunganisha Mungu kuwa mmoja kwani mmegawanya zaidi. Ingekuwa si kazi yangu ya upesiupesi kabla ya muda kuyoyoma, haijulikani mngeishi hivi kwa muda gani! Kuendelea kumgawanya Mungu namna hii, Anawezaje kuendelea kuwa Mungu wenu? Je, bado mngeendelea kumtambua Mungu? Je, bado mngemkiri Yeye kama baba yenu na mumrudie? Ningechelewa hata kidogo, inaonekana kwamba mngewarudisha “Baba na Mwana,” Yehova na Yesu kwenda Israeli na mdai kwamba nyinyi wenyewe ni sehemu ya Mungu. Kwa bahati nzuri, sasa ni siku za mwisho. Hatimaye, siku Niliyoitarajia kwa hamu imewadia, na ni baada tu ya kuifanya hatua hii ya kazi kwa mikono Yangu ndipo kumgawanya kwenu Mungu Mwenyewe kumesitishwa. Isingekuwa hivi, mngezidisha, hadi kuwaweka Mashetani wote miongoni mwenu kwenye meza zenu kwa ajili ya ibada. Hii ndiyo njama yenu! Mbinu yenu ya kumgawanya Mungu! Je, mtaendelea kufanya hivyo sasa? Hebu Niwaulize: Kuna Mungu Wangapi? Ni Mungu Yupi atawaletea wokovu? Je, ni Mungu wa kwanza, wa pili au wa tatu mnayemwomba? Ni nani kati Yao mnayemwamini? Je, ni Baba? Au ni Mwana? Au ni Roho? Niambie ni nani unayemwamini. Ijapokuwa kwa kila neno unasema unamwamini Mungu, mnachokiamini hasa ni akili zenu! Hamna Mungu mioyoni mwenu kabisa! Na bado akilini mwenu mna “Utatu Mtakatifu” kadhaa. Hamkubaliani na hili?

Ikiwa hatua tatu za kazi zitakadiriwa kulingana na dhana hii ya Utatu, basi ni lazima kuwe na Mungu watatu kwani kazi iliyofanywa na kila mmoja si sawa. Ikiwa yeyote miongoni mwenu anasema kwamba hakika Utatu upo, basi eleza huyu Mungu mmoja katika nafsi tatu ni nini hasa.

Baba Mtakatifu ni nini? Mwana ni nini? Roho Mtakatifu ni nini? Je, Yehova ni Baba Mtakatifu? Je, Yesu ni Mwana? Basi, Roho Mtakatifu je? Je, Baba si Roho? Je, kiini cha Mwana vilevile si Roho? Je, kazi ya Yesu haikuwa ya Roho Mtakatifu? Je, kazi ya Yehova haikufanywa wakati ule na Roho sawa tu na kazi ya Yesu? Mungu Anaweza kuwa na Roho wangapi? Kulingana na maelezo yako hizi nafsi tatu, yaani, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni mmoja; kama ni hivyo, kuna Roho watatu lakini kuwa na Roho watatu kunamaanisha kuwa kuna Mungu Watatu. Hii inamaanisha kuwa hakuna Mungu Mmoja wa kweli; Mungu wa aina hii anawezaje kuwa kiini asili cha Mungu? Kama unakubali kuwa kuna Mungu mmoja tu, basi Anawezaje kuwa na Mwana na awe Baba? Je, hizi si fikra zako mwenyewe? Kuna Mungu Mmoja tu, nafsi moja katika Mungu huyu, na Roho mmoja tu wa Mungu sawa tu na ilivyoandikwa katika Biblia kwamba “Kuna tu Roho Mtakatifu mmoja na Mungu mmoja tu.” Haijalishi kama Baba na Mwana unaowazungumzia wapo, kuna Mungu mmoja tu, na kiini cha Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu mnaowaamini ni kiini cha Roho Mtakatifu. Kwa maneno mengine, Mungu ni Roho, ila Ana uwezo wa kupata Mwili na kuishi miongoni mwa wanadamu na vilevile kuwa juu ya vitu vyote. Roho Wake anajumuisha kila kitu na Anapatikana kila mahala. Anaweza kuwa katika mwili na wakati huo huo awe ndani na juu ya ulimwengu. Kwa kuwa watu wanasema kwamba Mungu ndiye tu Mungu wa kweli, basi kuna Mungu mmoja, ambaye hawezi kugawanywa kwa mapenzi ya awaye yote! Mungu ni Roho mmoja tu, na nafsi moja; na huyo ni Roho wa Mungu. Ikiwa ni kama usemavyo, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, basi Hawa si watatu? Roho Mtakatifu ni kitu kimoja, Mwana ni kingine, na Baba vilevile ni kingine. Nafsi Zao ni tofauti na viini Vyao ni tofauti, iweje basi ziwe kila moja Yao ni sehemu ya Mungu mmoja? Roho Mtakatifu ni Roho; hili ni rahisi kueleweka kwa wanadamu. Ikiwa ni hivyo basi, Baba ni Roho zaidi. Hajawahi kushuka kuja duniani na Hajawahi kupata mwili; Yeye ni Yehova Mungu katika mioyo ya mwanadamu, na kwa hakika Yeye vilevile ni Roho. Basi kuna uhusiano gani kati Yake na Roho Mtakatifu? Je, ni uhusiano kati ya Baba na Mwana? Au ni uhusiano kati ya Roho Mtakatifu na Roho wa Mungu? Je, kiini cha kila Roho ni sawa? Au Roho Mtakatifu ni chombo cha Baba? Hili linaweza kuelezwaje? Aidha kuna uhusiano gani kati ya Mwana na Roho Mtakatifu? Je, ni uhusiano kati ya Roho wawili au ni uhusiano kati ya mwanadamu na Roho? Haya yote ni masuala ambayo hayawezi kuelezewa! Ikiwa Wote ni Roho mmoja, basi hapawezi kuwepo na mjadala kuhusu nafsi tatu, kwani zote zinamilikiwa na Roho mmoja. Kama Zingekuwa nafsi tofauti, basi Roho Zao Zingetofautiana katika nguvu zao na kamwe hawangekuwa Roho mmoja. Hii dhana ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni upuuzi mtupu! Hili linamweka Mungu katika vitengo na kumgawanya kuwa nafsi tatu, kila moja ikiwa na hadhi na Roho; basi Atawezaje kuwa Roho mmoja na Mungu mmoja? Hebu niambie, je, mbingu na dunia na vyote vilivyomo viliumbwa na Baba, Mwana, au na Roho Mtakatifu? Wengine husema Waliviumba kwa pamoja. Basi ni nani alimkomboa mwanadamu? Alikuwa Roho Mtakatifu,

Mwana, au Baba? Wengine husema ni Mwana aliyewakomboa wanadamu. Basi Mwana ni nani katika kiini? Siye kupata mwili kwa Roho wa Mungu? Mungu aliyepata mwili anamwita Mungu aliye Mbinguni Baba katika mtazamo wa mwanadamu aliyeumbwa. Je, hufahamu kuwa Yesu alizaliwa kutokana na utungaji mimba kupitia Roho Mtakatifu. Ndani yake mna Roho Mtakatifu; lolote usemalo, Yeye bado ni mmoja na Mungu wa Mbinguni, kwani Yeye ni kupata mwili kwa Roho wa Mungu. Hili wazo la Mwana si kweli Kabisa. Ni Roho mmoja anayefanya Kazi yote; Mungu Mwenyewe pekee, yaani, Roho wa Mungu anafanya kazi Yake. Roho wa Mungu ni nani? Je, si Roho Mtakatifu? Je, si Roho Mtakatifu anayefanya kazi ndani ya Yesu? Ingekuwa kazi haikufanywa na Roho Mtakatifu (yaani Roho wa Mungu), je, kazi Yake ingemwakilisha Mungu Mwenyewe? Yesu alipomwita Mungu wa mbinguni kwa jina la Baba alipokuwa akiomba, hili lilifanywa katika mitazamo ya mwanadamu aliyeumbwa, kwa sababu Roho wa Mungu alikuwa amevaa mwili wa kawaida na Alikuwa na umbile la nje la mwanadamu aliyeumbwa. Hata ikiwa ndani yake mlikuwa na Roho wa Mungu, umbo Lake la nje bado lilikuwa lile la mtu wa kawaida; kwa maana nyingine, Alikuwa “Mwana wa Adamu” jambo ambalo watu wote, akiwemo Yesu Mwenyewe, walilizungumzia. Na kwa sababu Anaitwa Mwana wa Adamu, Yeye ni mtu (Mwanamke au mwanamume, kwa vyovyote vile mwenye umbo la nje la mwanadamu) aliyezaliwa katika familia ya kawaida ya watu wa kawaida. Kwa hivyo, Yesu kumwita Mungu wa mbinguni kwa jina la Baba kulikuwa sawa na mlivyomwita mara ya kwanza Baba; Alifanya hivyo kutokana na mtazamo wa Mwanadamu aliyeumbwa. Je, mnakumbuka Sala ya Bwana ambayo Yesu aliwafundisha kukariri? “Baba Yetu Uliye mbinguni...” Aliwaambia wanadamu wote wamwite Mungu wa Mbinguni kwa jina la Baba. Na kwa kuwa Naye pia alimwita Baba, alifanya hivyo kutoka kwa mtazamo wa mtu aliye katika daraja moja nanyi nyote. Kwa kuwa mlimwita Mungu wa mbinguni Baba, hili linaonyesha kuwa Yesu alijichukulia kuwa katika daraja sawa nanyi, kama mwanadamu duniani aliyeteuliwa na Mungu (yaani, Mwana wa Mungu). Kama mnamwita Mungu “Baba,” je, hii si kwa sababu nyinyi ni wanadamu walioumbwa? Haijalishi Yesu alikuwa na mamlaka makubwa kiasi gani duniani, kabla ya kusulubiwa, Alikuwa tu Mwana wa Adamu, akiongozwa na Roho Mtakatifu (yaani, Mungu), Akiwa miongoni mwa viumbe wa duniani, kwani bado Alikuwa hajaikamilisha kazi Yake. Kwa hivyo, kumwita kwake Mungu wa mbinguni Baba kulikuwa tu unyenyekevu na utiifu Wake. Yeye kumwita Mungu (yaani, Roho aliye mbinguni) kwa namna ile, hata hivyo, hakudhibitishi kuwa Yeye ni Mwana wa Roho wa Mungu aliye mbinguni. Badala yake, ni kuwa mtazamo wake ni tofauti, si kwamba ni nafsi tofauti. Uwepo wa nafsi tofauti ni uongo. Kabla ya kusulubiwa kwake, Yesu alikuwa Mwana wa Adamu aliyefungwa katika udhaifu wa kimwili, na Hakuwa na mamlaka kamilifu ya Roho. Hiyo ndiyo maana Angeweza tu kutafuta mapenzi ya Mungu Baba kutoka katika mtazamo wa kiumbe. Ni kama tu Alivyoomba mara tatu huko Gethsemane: “Si kama Nitakavyo, bali kama Utakavyo.” Kabla Atundikwe msalabani, Hakuwa

zaidi ya Mfalme wa Wayahudi; alikuwa Kristo, Mwana wa Adamu, na wala si mwenye utukufu. Hiyo ndiyo maana, kutokana na mtazamo wa mwanadamu, Alimwita Mungu Baba. Sasa, huwezi kusema kuwa wote wamwitao Mungu Baba ni Wana. Ingekuwa kweli, basi wote si mngekuwa Mwana punde Yesu alipowafundisha Sala ya Bwana? Ikiwa bado hamjaridhika, basi niambieni hili, ni nani mmwitaye Baba? Ikiwa mnamrejelea Yesu, je, Baba ya Yesu ni nani kwenu? Baada ya Yesu kurudi mbinguni, hii dhana ya Baba na Mwana ilikoma. Hii dhana ilifaa tu kipindi ambacho Yesu alikuwa mwili; katika mazingira mengine yoyote, uhusiano ni ule wa kati ya Bwana wa uumbaji na kiumbe mnapomwita Mungu Baba. Hakuna wakati ambapo wazo hili la Utatu wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu linaweza kuwa na mashiko; ni uongo ambao ni nadra kuonekana na halipo!

Hili laweza kuwakumbusha watu maneno ya Mungu kutoka katika kitabu cha Mwanzo: “Na tumuumbe mwanadamu katika sura yetu, kwa mfanano wetu.” Ikichukuliwa kuwa Mungu anasema “na tumtengeneze” mtu kwa mfano “wetu,” basi “tu-” inaashiria wawili au wengi; na kwa kuwa anataja “tu-” basi hakuna tu Mungu mmoja. Kwa njia hii, mwanadamu alianza kufikiria udhahania wa nafsi bayana, na kutokana na maneno haya kulitokea dhana ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Basi, Baba anafananaje? Je, Mwana anafananaje? Na Roho Mtakatifu anafananaje? Yawezekana kuwa mwanadamu wa leo aliumbwa kwa mfano wa mtu mmoja aliyeunganishwa pamoja kutoka kwa nafsi tatu? Je, sura ya mwanadamu inafanana na ile ya Baba, Mwana, au Roho Mtakatifu? Mwanadamu ni mfano wa nani katika nafsi za Mungu? Mawazo ya mwanadamu ni ya kimakosa na upuuzi! Yanaweza tu Kungawanya Mungu kuwa Mungu kadhaa. Wakati Musa aliandika kitabu cha Mwanzo, ni baada ya wanadamu kuumbwa baada ya uumbaji wa dunia. Mwanzo kabisa, dunia ilipoanza, Musa hakuwepo. Ni hadi baadaye kabisa ndipo Musa aliandika Biblia, basi angejuaje alichokinena Mungu kutoka mbinguni? Hakuwa na ufahamu wowote jinsi Mungu alivyounda ulimwengu. Katika Agano la Kale la Biblia, hapakutajwa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, ni Mungu mmoja tu wa kweli, Yehova, akiifanya kazi yake nchini Israeli. Anaitwa majina tofauti kadri enzi zinavyobadilika, ila hili haliwezi kuthibitisha kuwa kila jina linarejelea mtu tofauti. Ingekuwa hivi, basi je, si kungekuwa na nafsi nyingi sana katika Mungu? Kilichoandikwa katika Agano la Kale ni kazi ya Yehova, hatua ya kazi ya Mungu Mwenyewe tangu mwanzo wa Enzi ya Sheria. Ilikuwa ni kazi ya Mungu, ambapo Alinena, ilikuwa, na Alipoamuru, ilitendeka. Hakuna hata wakati mmoja ambapo Yehova alisema kuwa alikuwa Baba aliyekuja kufanya kazi, wala Hakutabiri kuja kwa Mwana kuwakomboa wanadamu. Wakati wa Yesu ulipowadia, ilisemekana tu kwamba Mungu alikuwa Ameupata mwili kuwakomboa wanadamu, si kwamba ni Mwana aliyekuja amekuja. Kwa sababu enzi hazifanani na kazi ambayo Mungu Mwenyewe hufanya vilevile inatofautiana, Anapaswa kufanya kazi Yake katika milki tofauti, kwa njia hii utambulisho Alionao vilevile

unatofautiana. Mwanadamu anaamini kwamba Yehova ndiye Baba ya Yesu, ila hili halijakiriwa na Yesu ambaye alisema: “Hatukubainishwa kamwe kama Baba na Mwana; Mimi na Baba aliye Mbinguni ni kitu kimoja. Baba yu ndani Yangu Nami ni ndani Yake; wanadamu wanapomwona Mwana, wanamwona Baba.” Baada ya yote kusemwa, iwe Baba au Mwana, Wao ni Roho mmoja, Hawajagawanywa kuwa nafsi tofautitofauti. Mara tu wanadamu wanapojaribu kueleza, mambo hutatizwa na wazo la nafsi tofauti, na vilevile na uhusiano kati ya Baba, Mwana na Roho. Mwanadamu akizungumzia nafsi tofauti, je, hili halimfanyi Mungu kuwa kitu? Mwanadamu hata zaidi huziorodhesha nafsi hizi kama nafsi ya kwanza, ya pili, na ya tatu; haya yote ni mawazo ya mwanadamu yasiyofaa kurejelewa, hayana uhalisi kabisa! Ukimwuliza: “Kuna Mungu wangapi?” atasema kuwa Mungu ni Utatu Mtakatifu wa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu: Yule mmoja wa kweli. Ukiuliza tena: “Baba ni nani?” atasema: “Baba ni Roho wa Mungu aliye mbinguni; anatawala kila kitu, na kiongozi wa mbinguni.” “Je, Yehova ni Roho?” Atasema: “Ndiyo!” Ukimuuliza tena, “Mwana ni nani?” atasema kuwa Yesu ndiye Mwana, bila shaka. “Basi kisa cha Yesu ni kipi? Alitoka wapi?” Atasema: “Yesu alizaliwa na Maria kupitia kwa utungaji mimba wa Roho Mtakatifu.” “Je, kiini Chake si Roho vilevile? Je, kazi Yake si kiwakilishi cha Roho Mtakatifu? Yehova ni Roho, vivyo hivyo na kiini cha Yesu. Sasa katika siku za mwisho, bila shaka ni Roho Anayeendelea kufanya Kazi; Wangewezaje kuwa nafsi tofauti? Je, si Roho wa Mungu anafanya kazi ya Roho kutoka katika mitazamo tofauti?” Kwa hivyo, hakuna tofauti bayana kati ya nafsi. Yesu alipatikana kwa utungaji mimba wa Roho Mtakatifu, na bila shaka, Kazi Yake hasa ilikuwa ile ya Roho Mtakatifu. Katika hatua ya kwanza ya kazi iliyofanywa na Yehova, Hakuwa mwili au kuonekana kwa mwanadamu. Kwa hivyo mwanadamu hakuona uso Wake. Haijalishi Alikuwa mashuhuri au mrefu kiasi gani, bado Alikuwa Roho, Mungu Mwenyewe aliyemuumba mwanadamu mwanzoni. Yaani, alikuwa Roho wa Mungu. Aliponena na wanadamu kutoka mawinguni, alikuwa Roho tu. Hakuna hata mmoja aliyeuona Uso wake; ni katika Enzi ya Neema tu ambapo Roho wa Mungu alikuwa mwili na Alipata mwili kule Uyahudi ndipo mwanadamu aliona sura ya kupata mwili kama Myahudi. Hisia ya Yehova haingeweza kuhisika. Hata hivyo, Alipatikana kwa utungaji mimba wa Roho Mtakatifu, yaani, Alipatikana kwa utungaji mimba wa Roho wa Yehova Mwenyewe, na Yesu bado alizaliwa kama mfano halisi wa Roho wa Mungu. Alichokiona mwanadamu mwanzoni kilikuwa ni Roho Mtakatifu Akimshukia Yesu kama njiwa; Hakuwa Roho mwenye upekee kwa Yesu tu, badala yake alikuwa Roho Mtakatifu. Basi roho wa Yesu anaweza kutenganishwa na Roho Mtakatifu? Ikiwa Yesu ni Yesu, Mwana, na Roho Mtakatifu ni Roho Mtakatifu, basi wangewezaje kuwa kitu kimoja? Ingekuwa hivyo kazi isingefanywa. Roho ndani ya Yesu, Roho aliye mbinguni, na Roho wa Yehova wote ni mmoja. Anaweza kuitwa Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu, Roho aliyezidishwa mara saba, na Roho mwenye vyote. Roho wa Mungu anaweza kufanya kazi nyingi. Ana uwezo wa kuumba na kuiangamiza dunia kwa kuleta mafuriko duniani;

Anaweza kuwakomboa wanadamu, aidha, kuwashinda na kuwaangamiza wanadamu wote. Kazi hii yote inafanywa na Mungu Mwenyewe na haiwezi kufanywa na yeyote katika nafsi za Mungu kwa niaba Yake. Roho Wake anaweza kuitwa Yehova na Yesu, na vilevile mwenye Uweza. Yeye ni Bwana na Kristo. Anaweza pia kuwa Mwana wa Adamu. Yuko mbinguni na vilevile duniani; Yuko juu ya dunia na pia miongoni mwa umati. Yeye tu ndiye Bwana wa Mbingu na dunia! Tangu wakati wa uumbaji hadi sasa, kazi hii imekuwa ikifanywa na Roho wa Mungu Mwenyewe. Iwe ni kazi mbinguni au katika mwili, yote hufanywa na Roho Wake Mwenyewe. Viumbe wote, wawe mbinguni au duniani, wamo katika kiganja cha mkono Wake wenye nguvu; yote hii ni kazi ya Mungu na haiwezi kufanywa na yeyote kwa niaba Yake. Mbinguni Yeye ni Roho na vilevile Mungu Mwenyewe; miongoni mwa wanadamu, Yeye ni mwili ila anaendelea kuwa Mungu Mwenyewe. Japo Anaweza kuitwa mamia ya maelfu ya majina, Yeye bado ni Mungu Mwenyewe, na kazi yote ni maonyesho ya moja kwa moja ya Roho Wake. Ukombozi wa wanadamu wote kupitia kwa kusulubiwa Kwake ilikuwa kazi ya moja kwa moja ya Roho Wake, na vilevile tangazo kwa mataifa yote na nchi zote wakati wa siku za mwisho. Wakati wote Mungu anaweza kuitwa mwenye uweza na Mungu mmoja wa kweli, Mungu Mwenyewe mwenye vyote. Nafsi bayana hazipo, aidha dhana ya Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu haipo. Kuna Mungu mmoja mbinguni na duniani!

Mpango wa usimamizi wa Mungu umeenea katika miaka elfu sita na umegawanyika katika enzi tatu kutegemea tofauti katika kazi Yake: Enzi ya kwanza ni Enzi ya Sheria ya Agano la Kale; ya pili ni Enzi ya Neema; na ya tatu ni ile ya siku za mwisho—Enzi ya Ufalme. Katika kila enzi utambulisho tofauti huwasilishwa. Hili linafanywa kwa sababu ya utofauti wa kazi, yaani, mahitaji ya kazi. Hatua ya kwanza ya kazi wakati wa Enzi ya Sheria ilifanyiwa nchini Israeli, na hatua ya pili ya kuhitimisha kazi ya ukombozi ilifanyiwa Uyahudi. Kwa kazi ya ukombozi, Yesu alizaliwa kutokana na utungaji mimba wa Roho Mtakatifu na kama Mwana wa pekee. Haya yote yalitokana na mahitaji ya kazi. Katika siku za mwisho, Mungu anadhamiria kupanua kazi Yake katika watu wa Mataifa, na kuwashinda watu wa huko, ili kwamba jina lake liweze kuwa maarufu miongoni mwao. Anadhamiria kumwongoza mwanadamu katika kuelewa na kuingia katika ukweli wote. Kazi hii yote inafanywa na Roho mmoja. Ijapokuwa Anaweza kufanya hivyo kutoka mitazamo tofautitofauti, asili na kanuni za kazi zinabaki zile zile. Mara tu ukizifuata kanuni na asili ya kazi Waliyoifanya, basi utagundua kuwa yote ilikuwa kazi ya Roho mmoja. Hata hivyo, wengine wanaweza kusema: “Baba ni Baba; Mwana ni Mwana; Roho Mtakatifu ni Roho Mtakatifu, na mwishowe, Watafanywa kitu kimoja.” Je, Utawafanyaje kitu kimoja? Baba na Roho Mtakatifu Wawezaje kufanywa kitu kimoja? Ikiwa Walikuwa wawili kiasili, haijalishi Wamewekwa pamoja kwa namna gani, je, Hawataendelea kuwa sehemu mbili? Unaposema kuwa kuwafanya kuwa kitu kimoja, huko si kuunganisha sehemu mbili kutengeneza

kitu kamili? Je, Hawakuwa sehemu mbili kabla ya kufanywa kitu kizima? Kila Roho ana kiini kinachotofautiana, na Roho wawili Hawawezi kufanywa kuwa kitu kimoja. Roho si chombo cha kutengenezwa, si kama chombo chochote katika ulimwengu. Kulingana na mitazamo ya wanadamu, Baba ni Roho mmoja, Mwana ni mwingine, na Roho Mtakatifu tena ni mwingine, halafu Roho Hawa huchanganyika sawa na glasi tatu za maji kuunda kitu kimoja kizima. Je, hizo si sehemu tatu zimefanywa kuwa kitu kimoja? Haya bila shaka ni maelezo ya kimakosa! Je, huku si kumgawa Mungu? Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wanawezaje kufanywa kuwa kitu kimoja? Je, Wao si sehemu tatu zenye asili tofauti? Aidha kuna wale wasemao, “je, si Mungu alitaja wazi kuwa Yesu ni Mwanawe mpendwa?” Yesu ni Mwana mpendwa wa Mungu, ambaye anapendezwa naye—haya bila shaka yalitamkwa na Mungu Mwenyewe. Huyu alikuwa Mungu akijitolea ushuhuda Mwenyewe, ila kutoka katika mtazamo tofauti, ule wa Roho aliye mbinguni akitolea ushuhuda kupata Mwili Kwake. Yesu ni kupata mwili Kwake, si Mwanake mbinguni. Je, unaelewa? Je, maneno ya Yesu, “Mimi ni ndani ya Baba naye Baba yu ndani yangu,” hayaonyeshi kuwa Wao ni Roho mmoja? Na si kwa sababu ya kupata mwili kulikosababisha kutenganishwa Kwao kati ya mbinguni na duniani? Uhalisi ni kwamba Wao ni kitu kimoja; hata iweje, ni Mungu anajitolea ushuhuda Mwenyewe. Kutokana na kubadilika kwa enzi, mahitaji ya kazi, na hatua mbalimbali za mpango Wake wa usimamizi, vilevile jina wamwitaleo wanadamu hubadilika. Alipokuja kufanya hatua ya kwanza ya kazi, Angeweza kuitwa tu Yehova, mchungaji wa Waisraeli. Katika hatua ya pili, Mungu mwenye mwili Angeweza kuitwa tu Bwana, na Kristo. Lakini wakati huo, Roho aliye mbinguni alikariri tu kwamba Alikuwa Mwana mpendwa wa Mungu, bila kutaja kuwa Alikuwa Mwana wa pekee wa Mungu. Hili halikufanyika kabisa. Mungu angewezaje kuwa na Mwana wa pekee? Basi, Mungu asingekuwa mwanadamu? Kwa kuwa Alikuwa Mwili, Aliitwa Mwana mpendwa wa Mungu na kutokana na hili, kukazuka uhusiano wa Baba na Mwana. Ni kwa sababu tu ya utengano kati ya mbingu na dunia. Yesu aliomba kutokana na msimamo wa mwili. Kwa sababu Alikuwa Amapata mwili wa ubinadamu wa kawaida, ni kutokana na msimamo wa mwili ndipo Alisema: “Umbo Langu la nje ni la kiumbe. Kwa sababu Nilijivisha mwili kuja duniani, sasa Niko mbali, mbali sana na mbinguni.” Kwa sababu hii, Angeomba tu kwa Baba kutokana na msimamo wa mwili. Huu ulikuwa wajibu Wake, ambao ni sharti Roho wa Mungu aliyepata mwili anapaswa kupewa. Haiwezekani kusema kwamba Hawezi kuwa Mungu kwa sababu tu Anamwomba Baba kutokana na msimamo wa mwili. Ijapokuwa Anaitwa Mwana mpendwa wa Mungu, Yeye bado ni Mungu Mwenyewe, ni vile tu Yeye ni mwili wa Roho, na kiini chake bado ni Roho. Kama wanavyoona wanadamu, wanashangaa ni kwa nini Anaomba ikiwa yeye ni Mungu Mwenyewe. Hii ni kwa sababu Yeye ni Mungu mwenye mwili, Mungu aishiye mwilini, bali si Roho aliye mbinguni. Kama anavyoona mwanadamu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wote ni Mungu. Ni kwamba tu wote watatu wanafanywa kuwa kitu kimoja na kudhaniwa kuwa Mungu wa Kweli, na kwa njia hii,

uwezo Wake unakuwa mkuu kupindukia. Kuna wanaosema kuwa ni kwa njia hii tu anakuwa Roho aliyezidishwa mara saba. Mwana alipoomba baada ya kuja Kwake, alimwomba Roho. Kwa hakika, alikuwa Akiomba kutokana na msimamo wa kiumbe. Kwa kuwa mwili si kamili, Hakuwa mkamilifu na pia Alikuwa na udhaifu mwingi Alipokuja katika mwili, na Alisumbuka sana Alipoifanya kazi Yake katika mwili. Hii ndiyo maana Alimwomba Mungu Baba mara tatu kabla ya kusulubiwa Kwake, na hata mara nyingi zaidi kabla ya hapo. Aliomba miongoni mwa wanafunzi Wake; Aliomba peke Yake juu mlimani; Aliomba Akiwa Ameabiri dau la uvuvi; Aliomba Akiwa katika umati; Aliomba akiwa anaumega mkate; na kuomba akiwa Anawabariki wengine. Kwa nini Alifanya hivyo? Ilikuwa ni Roho Aliyemwomba; Alikuwa Akimwomba Roho, Alimwomba Mungu aliye mbinguni; kutokana na msimamo wa mwili. Hivyo basi kutoka katika msimamo wa mwanadamu, Yesu alikuwa Mwana katika hatua ile ya kazi. Katika hatua hii hata hivyo, Haombi. Kwa nini? Hii ni kwa sababu Anachokileta ni kazi ya neno, na hukumu na kuadibu kutumia neno. Hana haja ya maombi na huduma Yake ni ya kunena. Hajawekwa msalabani, na hashitakiwi na wanadamu kwa wale walio madarakani. Anafanya tu kazi Yake na yote yanakuwa sawa. Wakati Yesu alipoomba, Alikuwa akimwomba Mungu Baba ili ufalme wa mbinguni ushuke, ili mapenzi ya Baba yatimizwe, na ili kazi ifike. Katika hatua hii, ufalme wa mbinguni umeshuka, basi, Ana haja ya kuendelea kuomba? Kazi Yake ni kuihitimisha enzi, na hakuna tena enzi mpya, basi, kuna haja ya kuombea hatua inayofuata? Ninasikitika hakuna haja!

Kuna ukinzani mwingi katika maelezo ya mwanadamu. Kweli, haya ni mawazo ya mwanadamu; bila uchunguzi zaidi, ambayo nyote mngeamini kuwa yako sahihi. Je, hamjui hii dhana ya Mungu kama Utatu Mtakatifu ni mawazo ya mwanadamu tu? Hakuna ufahamu wa mwanadamu ulio mzima na kamili. Mara zote kuna madoa, na mwanadamu ana mawazo mengi mno; hili linaonyesha kuwa kiumbe hawezi kuieleza kazi ya Mungu. Kuna mengi sana katika akili ya mwanadamu, yote yakitokana na mantiki na tafakari, ambayo hukinzana na ukweli. Je, mantiki yako yaweza kuichangua kazi ya Mungu? Je, waweza kupata utambuzi wa kazi yote ya Yehova? Je, ni wewe kama mwanadamu uwezaye kubaini yote, au ni Mungu Mwenyewe awezaye kuona kutoka milele hadi milele? Je, ni wewe mwanadamu uwezaye kuona tangu milele ya zamani sana hadi milele ijayo, au Mungu ndiye Ana uwezo wa kufanya hivyo? Unasema nini? Unafaa vipi kumweleza Mungu? Maelezo yako yametegemezwa katika misingi gani? Wewe ni Mungu? Mbingu na dunia, na vyote vilivyomo viliumbwa na Mungu Mwenyewe. Si wewe uliyelifanya hili, basi ni kwa nini unatoa maelezo yasiyo sahihi? Sasa, unaendelea kuamini katika utatu mtakatifu? Hufikirii kuwa huu ni mzigo mkubwa kwa njia hii? Itakuwa bora kwako kuamini katika Mungu mmoja, si watatu. Ni bora zaidi kuwa mwepesi, kwani mzigo wa Bwana ni mwepesi.

Utendaji (3)

Lazima muwe na uwezo wa kuishi kwa kujitegemea, wa kula na kunywa maneno ya Mungu ninyi wenyewe, kupitia maneno ya Mungu ninyi wenyewe, na kuishi maisha ya kawaida ya kiroho bila uongozi wa wengine. Lazima muweze kuyategemea maneno ambayo Mungu ananena leo ili muishi, ili muingie katika uzoefu wa kweli, na kupata umaizi wa kweli. Ni kwa kufanya hivi tu ndiyo mtaweza kusimama imara. Leo, watu wengi hawaelewi kikamilifu majonzi na majaribu ya siku za usoni. Katika siku za usoni, watu wengine watapitia majonzi, na wengine watapitia adhabu. Adhabu hii itakuwa kali zaidi; itakuwa ni kuwasili kwa ukweli. Leo, yote unayopitia, kutenda, na kuonyesha yanaweka msingi wa majaribu ya siku za usoni, na kwa kiwango cha chini mno, lazima uweze kuishi kwa kujitegemea. Leo, hali inayohusu wengi kanisani ni kama ifuatayo kwa jumla: Ikiwa kuna viongozi na wafanyakazi wa kufanya kazi hiyo, wao huwa na furaha, na ikiwa hawapo, wao hukosa furaha. Wao hawatilii maanani kazi ya kanisa, wala kwa maisha yao wenyewe ya kiroho, na hawana hata mzigo kidogo kabisa—wao huboronga tu kama ndege wa Hanhao.^[a] Kusema kweli, ndani ya watu wengi kazi ambayo Nimefanya ni kazi ya ushindi tu, kwani wengi hawastahili kimsingi kufanywa wakamilifu. Ni sehemu ndogo tu ya watu ndio wanaweza kufanywa wakamilifu. Ikiwa, baada ya kuyasikia maneno haya, unawaza “kwa kuwa kazi inayofanywa na Mungu ni kwa ajili tu ya kuwashinda watu, nitafuata tu kwa uzembe,” mwelekeo wa aina hiyo ungewezaje kukubalika? Ikiwa kweli unamilikiwa na dhamiri, basi lazima uwe na mzigo, na hisia ya kuwajibika. Lazima useme: “Iwe nitashindwa au kufanywa mkamilifu, lazima niwe na hatua hii ya ushuhuda kwa kufaa.” Kama kiumbe wa Mungu, mtu anaweza kushindwa kabisa na Mungu, na hatimaye, mtu anakuwa na uwezo wa kumridhisha Mungu, kulipa upendo wa Mungu kwa moyo wenye upendo kwa Mungu na kwa kujitolea mwenyewe kabisa kwa Mungu. Hili ni jukumu la mwanadamu, ni wajibu unaopaswa kutekelezwa na mwanadamu, na ni mzigo unaopaswa kubebwa na mwanadamu, na mwanadamu lazima atimize agizo hili. Ni wakati huo tu ndipo atakuwa anaamini katika Mungu kwa hakika. Leo, kile unachofanya kanisani ni timizo la wajibu wako? Hili linategemea na kama umebeba mzigo, na inategemea maarifa yako mwenyewe. Katika kuipitia kazi hii, ikiwa mwanadamu anashindwa na ana maarifa ya kweli, basi ataweza kutii bila kujali matarajio au majaliwa yake mwenyewe. Kwa njia hii, kazi kuu ya Mungu itafanywa yote kabisa, kwani ninyi watu hamwezi kufanya lolote zaidi ya hili, na hamwezi kutimiza mahitaji yoyote ya juu zaidi. Ihali katika siku za usoni, watu wengine watafanywa wakamilifu. Ubora wao wa tabia utakuwa mzuri zaidi, ndani ya roho zao watakuwa na maarifa ya kina zaidi, na maisha yao yatakua.... Ihali wengine hawawezi kabisa kulitimiza hili, na hivyo hawawezi kuokolewa. Kuna sababu ya Mimi kusema kwamba hawawezi kuokolewa. Katika siku za usoni, wengine watashindwa, wengine wataondoshwa, wengine watafanywa wakamilifu, na wengine watatumiwa—na kwa

hiyo wengine watapitia majonzi, wengine watapitia adhabu (majanga ya asilia pamoja na misiba inayosababishwa na mwanadamu), wengine wataondoshwa, na wengine watasalia. Katika hili, kila mmoja ataainishwa kulingana na aina, na kila kikundi kikiwakilisha aina ya mtu. Sio watu wote wataondoshwa, wala watu wote kufanywa wakamilifu. Hili ni kwa sababu ubora wa tabia wa watu wa China ni duni sana, na kuna idadi ndogo tu miongoni mwao walio na aina ya kujitambua ambayo Paulo alikuwa nayo. Miongoni mwenu, wachache wana azimio la kumpenda Mungu sawa na alilokuwa nalo Petro, au imani ya aina sawa na aliyokuwa nayo Ayubu. Kuna wachache sana kati yenu wanaomcha na kumtumikia Yehova kama alivyofanya Daudi, wale walio na kiwango sawa cha uaminifu. Mnasikitisha jinsi gani!

Leo, mazungumzo juu ya kufanywa mkamilifu ni kipengele kimoja tu. Haijalishi kinachofanyika, lazima muwe na hatua hii ya ushuhuda kwa kufaa. Kama mungeulizwa mumhudumie Mungu katika hekalu, mngefanyaje hivyo? Kama hungekuwa kuhani, na hungekuwa na cheo cha wana wazaliwa wa kwanza au wana wa Mungu, bado ungeweza kuwa mwaminifu? Bado ungeweza kutumia juhudi zako katika kazi ya kuupanua ufalme? Bado ungeweza kufanya kazi ya agizo la Mungu inavyofaa? Haijalishi jinsi ambavyo maisha yako yamekua, kazi ya leo itakusababisha uridhishwe kabisa ndani yako, na uweke kando fikira zako zote. Kama kile una kinachohitajika kuyafuatilia maisha au la, kazi ya Mungu itakufanya uridhike kabisa. Watu wengine husema: “Naamini katika Mungu, na sielewi ni nini maana ya kuyafuatilia maisha.” Na wengine husema: “Mimi nimetatanishwa katika imani yangu kwa Mungu. Najua kwamba siwezi kufanywa mkamilifu, kwa hivyo niko tayari kuadibiwa.” Hata watu kama hawa, ambao wako tayari kuadibiwa au kuangamizwa, lazima washurutishwe kukubali kwamba kazi ya leo inafanywa na Mungu. Watu wengine pia husema: “Siombi kufanywa mkamilifu, lakini, leo, niko radhi kukubali mafundisho yote ya Mungu, na niko radhi kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida, kuendeleza ubora wa tabia yangu, na kutii mipango yote ya Mungu....” Katika hili, wao pia wameshindwa na kuwa na ushuhuda, ambalo linathibitisha kwamba kuna maarifa fulani kuhusu kazi ya Mungu ndani ya watu hawa. Hatua hii ya kazi imetekelezwa haraka kabisa, na katika siku za usoni, itatekelezwa hata kwa haraka zaidi huko ng’ambo. Leo, watu walio ng’ambo hawawezi kungoja, wote wanakimbilia Uchina—na kwa hiyo ikiwa hamwezi kufanywa wakamilifu, mtakuwa mnawashikilia watu walio ng’ambo. Wakati huo, haijalishi mumeingia vizuri kwa namna gani au jinsi mliyoy, wakati utakapofika kazi Yangu itahitimishwa na kutimizwa. Kazi Yangu haitacheleweshwa na ninyi. Nafanya kazi ya wanadamu wote, na hakuna haja ya Mimi kutumia muda wowote zaidi kwenu! Ninyi ni msio na motisha kabisa, mnaokosa kujitambua kabisa! Hamstahili kufanywa wakamilifu—mna uwezo mdogo sana! Katika siku za usoni, hata watu wakiendelea kuwa wazembe na hobelahobela sana, na kubaki wasioweza kuboresha ubora wao wa tabia, hili halitazuia kazi ya ulimwengu mzima.

Wakati ukifika wa kazi ya Mungu kumalizika, itamalizika, na wakati ukifika wa watu kuondoshwa, wataondoshwa. Bila shaka, wale wanaopaswa kufanywa wakamilifu, na wanastahili kufanywa wakamilifu, pia watafanywa wakamilifu—lakini ikiwa hamna tumaini kabisa, basi kazi ya Mungu haitawangoja ninyi! Hatimaye, ukishindwa, hili pia linaweza kufikiriwa kama kuwa na ushuhuda. Kuna mipaka kwa kile ambacho Mungu anahitaji kutoka kwenu; urefu ule wa kimo ambacho mwanadamu anaweza kutimiza ndio, urefu wa ushuhuda unaotakiwa kutoka kwake. Sio kama anavyofikiria mwanadamu kwamba ushuhuda kama huo utafikia mipaka ya juu zaidi na kwamba utakuwa mkubwa sana—hakuna vile ambavyo hili linaweza kutimizwa ndani ya ninyi watu wa China. Nimeshirikiana nanyi kwa wakati huu wote, na ninyi wenyewe mmeona hili: Nimewaambia msipinge, msiwe waasi, msifanye mambo yanayosababisha usumbufu au yanayovuruga bila Mimi kufahamu. Nimewakosoa watu moja kwa moja kuhusu hili mara nyingi, lakini hata hilo halitoshi—punde tu wanapogeuka wao hubadilika, huku wengine hunipinga Mimi kisirisiri, bila majuto yoyote. Unadhani sijui lolote kuhusu hili? Unadhani unaweza kunisababishia Mimi matatizo na hakuna kitakachotokea? Unadhani sijui unapojaribu kubomoa kazi Yangu bila Mimi kufahamu? Unadhani kwamba hila zako ndogo zinaweza kushikilia nafasi ya hulka yako? Wewe kila mara unaonekana kuwa mtiifu lakini wewe ni mdanganyifu kisirisiri, unaficha mawazo mabaya ndani ya moyo wako, na hata kifo si adhabu ya kutosha kwa watu kama wewe! Unadhani kwamba kazi kidogo inayofanywa na Roho Mtakatifu ndani yako inaweza kuchukua nafasi ya uchaji wako Kwangu? Unafikiri ulipata nuru kupitia kwa kuiita Mbinguni? Wewe huna aibu! Wewe huna thamani kabisa! Unafikiria kwamba “matendo yako mema” yalikuwa ya kuigusa Mbinguni sana, na kwamba kwa sababu hiyo Alifanya jambo la pekee na kukupa kiasi kidogo cha vipawa, vilivyokufanya uwe na lugha ya kushawishi, iliyokukubalia kuwadanganya wengine, na kunidanganya Mimi? Wewe ni mpumbavu kweli! Je, wajua mahali ambapo nuru yako inatoka? Je, hujui ulikula chakula cha nani ulipokuwa unakua? Wewe ni wa kupita kiasi kweli! Wengine miongoni mwenu hawajabadilika hata baada ya miaka minne au mitano ya kushughulikiwa na mnaelewa kuhusu mambo haya. Mnapaswa kuelewa asili yenu, na msipinge wakati ambapo, siku moja, mtatelekezwa. Wengine, ambao hudanganya wale walio juu na walio chini yao katika huduma yao, wameshughulikiwa sana; wengine, kwa sababu ni wenye tamaa ya pesa, wameshughulikiwa kwa kiasi kikubwa; wengine, kwa sababu hawaweki mipaka iliyo wazi baina ya wanaume na wanawake, pia wameshughulikiwa mara kwa mara; wengine kwa sababu ni wavivu, wanaofikiria tu juu ya mwili, na hawatendi kulingana na kanuni wanapotenda makanisa, wameshughulikiwa kwa kiasi kikubwa; wengine kwa sababu wao hukosa kuwa na ushuhuda popote waendapo, na hutenda kwa ukaidi na purukushani, na hata kufanya dhambi kwa makusudi, wameonywa mara nyingi kuhusu hili; wengine ambao huzungumza tu kuhusu maneno na mafundisho wakati wa mikutano, wakijiona kuwa wa cheo cha juu kuliko wengine wote,

wakikosa uhalisi hata kidogo kabisa wa ukweli, na kupanga njama dhidi ya kina ndugu na kupingana nao—wamefichuliwa mara kwa mara kwa sababu ya hili. Nimezungumza maneno haya kwenu mara nyingi sana, na leo, Sitazungumza tena kuhusu hili—fanyeni mtakalo! Fanyeni uamuzi wenu wenyewe! Watu wengi hawajapitia kushughulikiwa kwa namna hii kwa mwaka mmoja au miwili tu, kwa wengine imekuwa miaka mitatu au minne, huku wengine wamepitia hili kwa zaidi ya muongo mmoja, wakiwa wamepitia kushughulikiwa walikuwa waumini, lakini kufikia sasa kumekuwa na mabadiliko madogo ndani yao. Unasemaje nini, wewe sio kama nguruwe? Inaweza kuwa kwamba Mungu anawaonea? Usifikiri kwamba kazi ya Mungu haitamalizika ikiwa hamwezi kufikia kiwango fulani. Je, Mungu bado atawangoja ikiwa hamwezi kutimiza matakwa Yake? Nawaambia waziwazi—hali si hivyo tena! Usiwe na mtazamo kama huo wa kutia matumaini kuhusu mambo! Kuna kipimo kwa kazi ya leo hii, na Mungu hachezi tu na wewe! Hapo awali, ilipofikia kupitia jaribu la watendaji huduma, watu walifikiri kwamba kwa wao kusimama imara katika ushuhuda wao kwa Mungu na kushindwa na Yeye, walitakiwa kufikia kiwango fulani—walitakiwa kuwa watendaji huduma kwa hiari na kwa furaha, na walitakiwa kumsifu Mungu kila siku, na wasiwe wajeuri au wenye harara hata kidogo. Walifikiri kwamba ni wakati huo tu ndipo wangukuwa watendaji huduma kweli, lakini hali ni hiyo kwa kweli? Wakati huo, watu wa aina mbali mbali walifichuliwa; walionyesha tabia za kila aina. Wengine walitoa malalamiko, wengine walikuwa na fikira, wengine waliacha kuhudhuria mikutano, na wengine hata waligawa pesa za kanisa. Kina ndugu walikuwa wakila njama dhidi ya wengine. Ulikuwa ukombozi mkubwa kweli, lakini kulikuwa na kitu kimoja kizuri kulihusu: Hakuna aliyerudi nyuma. Hii ndiyo iliyokuwa hoja kubwa zaidi. Walikuwa na hatua ya ushuhuda mbele ya Shetani kwa sababu ya hili, na baadaye walipata utambulisho wa watu wa Mungu na wamefaulu hata kufikia leo. Kazi ya Mungu haitekelezwi unavyofikiria, badala yake, muda ukiisha, kazi hiyo itaisha, bila kujali umefikia hatua gani. Watu wengine huenda wakasema: “Kwa kutenda hivi Huwaokoi watu, au kuwapenda—Wewe si Mungu mwenye haki.” Nakwambia waziwazi: Kiini cha kazi Yangu leo ni kukushinda wewe na kukufanya uwe na ushuhuda. Kukuokoa wewe ni nyongeza tu; kama unaweza kuokolewa au la hutegemea ufuatiliaji wako mwenyewe, na hakuhusiani na Mimi. Ilhali lazima Nikushinde wewe; usijaribu kila mara kunidhibiti Mimi—leo Ninakufinyanga na kukuokoa, si vinginevyo!

Leo, kile ambacho mmepata kuelewa ni cha juu zaidi kuliko kile cha mtu yeyote kote katika historia ambaye hakufanywa mkamilifu. Iwe ni ufahamu wenu wa majaribu au imani katika Mungu, vyote ni vya juu zaidi kuliko ya muumini yeyote katika Mungu. Mambo mnayoyafahamu ni yale mnayokuja kujua kabla ya ninyi kupitia majaribu ya mazingira, lakini kimo chenu halisi hakipatani nayo. Kile mnachojua ni cha juu zaidi kuliko kile mnachotia katika vitendo. Ingawa mnasema kwamba watu wanaoamini katika Mungu wanapaswa kumpenda

Mungu, na hawapaswi kupania baraka bali kuyaridhisha tu mapenzi ya Mungu, kinachoonekana katika maisha yenu ni tofauti kabisa na hili, na kimewekwa mawaa kabisa. Watu wengi huamini katika Mungu kwa ajili ya amani na manufaa mengine. Isipokuwa kwa manufaa yako, wewe huamini katika Mungu, na ikiwa huwezi kupokea neema za Mungu, wewe huanza kununa. Kile ambacho umesema kingekuwaje kimo chako halisi? Inapofikia matukio ya familia yasiyoepukika kama vile watoto kuwa wagonjwa, wependwa kulazwa hospitalini, mazao mabaya ya mimea, na kuteswa na watu wa familia, hata mambo haya yanayotokea mara kwa mara, ya kila siku yanakuwa ya kukithiri kwako. Wakati ambapo mambo hayo hufanyika, wewe huingia katika hofu kubwa, hujui la kufanya—na wakati mwingi, wewe hulalamika kuhusu Mungu. Wewe hulalamika kwamba maneno ya Mungu yalikuhadaa, kwamba kazi ya Mungu yalikudhihaki. Je, ninyi hamna mawazo kama haya? Unadhani mambo kama haya hufanyika miongoni mwenu mara chache tu? Mnatumia kila siku kuishi katikati ya matukio kama haya. Hamfikirii hata kidogo sana kuhusu mafanikio ya imani yenu katika Mungu, na namna ya kuyaridhisha mapenzi ya Mungu. Kimo chenu halisi ni kidogo sana, hata kidogo zaidi kuliko cha kifaranga mdogo. Wakati ambapo biashara ya familia zenu hupoteza pesa ninyi hulalamika kuhusu Mungu, wakati ambapo ninyi hujikuta katika mazingira yasiyo na ulinzi wa Mungu ninyi bado hulalamika kuhusu Mungu, na ninyi hulalamika hata wakati ambapo mmoja wa vifaranga wenu hufa au ng'ombe mzee ndani ya zizi anapougua. Ninyi hulalamika kama ni wakati wa wana wenu kufunga ndoa lakini familia yenu haina pesa za kutosha; unataka kutekeleza kazi ya kanisa ya kuwa mwenyeji, lakini huwezi kuimudu, na kisha wewe hulalamika pia. Umejawa na malalamiko, na wakati mwingine huhudhuria mikutano au kula na kunywa maneno ya Mungu kwa sababu ya hili, wakati mwingine wewe huishia kuwa hasi kwa muda mrefu sana. Hakuna chochote kinachokufanyikia leo hii kilicho na uhusiano wowote na matazamio au majaliwa yako; mambo haya yangeanyika pia hata ikiwa hungeamini katika Mungu, ilhali leo hii unampitishia Mungu wajibu wa haya mambo, na kuisitiza kusema kwamba Mungu amekuondosha wewe. Na kuhusu imani yako katika Mungu, je? Umeyatoa maisha yako kwa kweli? Mngepitia majaribu sawa na yale ya Ayubu, hakuna hata mmoja miongoni mwenu anayemfuata Mungu leo hii angeweza kusimama imara, nyote mngeanguka chini. Na kunayo, kawaida kabisa, tofauti kubwa kati ya ninyi na Ayubu. Leo, kama nusu ya mali yenu ingetwaliwa mngethubutu kukana kuwepo kwa Mungu; kama mtoto wenu wa kiume au wa kike angechukuliwa kutoka kwenu, mngekimbia barabarani mkilalamika vikali; kama njia yako ya pekee kupata riziki ingegonga mwamba, ungejaribu kuanza kujadiliana mada hiyo na Mungu; ungeuliza kwa nini Nilisema maneno mengi sana hapo mwanzo kukutisha wewe. Hakuna kitu chochote ambacho hamngethubutu kufanya katika nyakati kama hizi. Hili linaonyesha kwamba hamjapata umaizi wowote wa kweli, na hamna kimo cha kweli. Hivyo, majaribu yaliyo ndani yenu ni makubwa mno, kwani ninyi mnajua mengi sana, lakini kile mnachoelewa kweli si hata sehemu moja kwa elfu ya kile

mnachofahamu. Msikome tu kwa ufahamu na maarifa pekee; mngeona vyema kiasi gani mnachoweza kutia katika vitendo kwa kweli, kiasi gani cha nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu kilipatikana kupitia katika jasho la bidii yenu wenyewe, na katika matendo mangapi yenu mmetambua azimio lenu wenyewe. Unapaswa kuchukua kimo chako na kutenda kwa uzito. Katika imani yako kwa Mungu, hupaswi tu kujaribu kufanya mambo kwa namna isiyo ya dhati kwa ajili ya yeyote—kama unaweza hatimaye kupata ukweli na uzima au la hutegemea ufuatiliaji wako mwenyewe.

Tanbihi:

a. Hadithi ya ndege wa Hanhao inafanana sana na hekaya ya Aesop ya mchwa na panzi. Ndege wa Hanhao anapendelea kulala badala ya kujenga kiota wakati hali ya hewa ni ya vuguvugu—liche ya maonyo ya tena na tena kutoka kwa jirani yake, ndege wa jamii ya kunguru. Wakati ambapo majira ya baridi kali hufika, ndege huyo huona baridi sana hadi kufa.

Utendaji (4)

Amani na furaha Nizungumziayo leo sio sawa na kile ambacho unaamini na kufahamu. Ulikuwa ukifikiri kwamba amani na furaha yalimaanisha kuwa na furaha siku nzima, kutokuwako kwa magonjwa au misiba katika familia yako, kuwa mwenye furaha kila mara ndani ya moyo wako bila hisia hata kidogo za huzuni, na kuwa na furaha isiyoelezeka bila kujali kiasi ambacho maisha yako yamekua. Hilo lilikuwa ni pamoja na kupata nyongeza na mwanao kuingia katika chuo kikuu karibuni. Ukiwa unayafikiria mambo haya, ulimwomba Munguna, ulipoona kwamba neema ya Mungu ilikuwa kuu sana, ulikuwa na furaha sana, ukitabasamu kutoka sikio hadi sikio, na hungeacha kumshukuru Mungu. Amani na furaha kama hiyo siyo ndiyo amani na furaha halisi itokanayo na kuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu. Badala yake, ni amani na furaha itokanayo na kuridhika kwa mwili. Unapaswa kufahamu enzi ya leo ni gani; siyo Enzi ya Neema, na si tena wakati ambapo unatafuta kulijaza tumbo lako kwa mkate. Unaweza kufurahi mno kwa sababu mambo yote yanaendelea vyema katika familia yako, lakini maisha yako yamo katika hali mahututi—na hivyo, haijalishi vile furaha yako ilivyo kuu, Roho Mtakatifu hayuko nawe. Kupata uwepo wa Roho Mtakatifu ni rahisi: fanya unachopaswa kufanywa kwa kufaa, tekeleza wajibu na kazi ya binadamu vizuri, na uweze kujiandaa na vitu unavyohitaji ili kufidia upungufu wako. Ikiwa kila mara una mzigo kwa ajili ya maisha yako na unafurahi kwa sababu umetambua ukweli au umefahamu kazi ya Mungu ya sasa, huku kweli ni kuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu. Au, iwapo wakati mwingine unapatwa na wasiwasi kwa sababu unapitia tatizo fulani ambalo hujui namna ya kulipitia, au kwa sababu huelewi ukweli unaoshirikiwa, hili linathibitisha kwamba Roho Mtakatifu yuko nawe. Hizi ni hali za kawaida katika tukio la uzoefu wa maisha. Lazima uelewe tofauti kati ya kuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu na kuukosa, na usiwe wa kawaida mno katika mtazamo wako wa hili.

Hapo awali, ilisemwa kwamba kuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu na kuwa na kazi ya Roho Mtakatifu ni tofauti. Hali ya kawaida ya kuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu inadhihirishwa katika kuwa na mawazo ya kawaida, mantiki ya kawaida, na ubinadamu wa kawaida. Tabia ya mtu itabaki kama ilivyokuwa, lakini ndani yake kutakuwa na amani, na nje atamstahi mtakatifu. Hivi ndivyo atakavyokuwa wakati ambapo Roho Mtakatifu yuko naye. Wakati ambapo mtu yuko na uwepo wa Roho Mtakatifu, kufukiria kwake ni kwa kawaida. Anapokuwa na njaa yeye hutaka chakula, anapona kiu yeye hutaka kunywa maji. ... Udhihirisho kama huu wa ubinadamu wa kawaida si nuru kutoka kwa Roho Mtakatifu; ni kufikiria kwa kawaida kwa watu na hali ya kawaida ya kuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu. Watu wengine huamini kimakosa kwamba wale walio na uwepo wa Roho Mtakatifu huwa hawaoni njaa, kwamba huwa hawahisi uchovu, na huwa hawaifikirii familia, wakiwa takribani wamejitenga kabisa kutoka kwa mwili. Kwa kweli, kadiri Roho Mtakatifu alivyo na watu, ndivyo wanavyokuwa wa kawaida zaidi. Wanajua kuteseka na kujitolea kwa ajili ya Mungu, kujitumia kwa ajili ya Mungu, na kuwa waaminifu kwa Mungu; zaidi ya hayo, wao hufikiria kuhusu chakula na mavazi. Kwa maneno mengine, hawajapoteza chochote cha ubinadamu wa kawaida wanachopaswa kuwa nacho na, badala yake, wanakuwa hasa na mantiki. Wakati mwingine, wao husoma maneno ya Mungu na kuitafakari kazi ya Mungu; kuna imani ndani ya mioyo yao na wako radhi kufuatilia ukweli. Kwa kawaida, kazi ya Roho Mtakatifu inategemewa juu ya msingi huu. Kama watu hawana fikira za kawaida, basi hawana mantiki—hii si hali ya kawaida. Watu wanapokuwa na fikira za kawaida na Roho Mtakatifu yuko nao, hakika wao huwa na mantiki ya mtu wa kawaida na hivyo, wao huwa na hali ya kawaida. Katika kupitia kazi ya Mungu, kuwa na kazi ya Roho Mtakatifu hutokea mara chache, ilhali uwepo wa Roho Mtakatifu uko takribani nyakati zote. Maadamu mantiki na fikira za watu ni za kawaida, na maadamu hali zao ni za kawaida, basi Roho Mtakatifu yuko nao kwa hakika. Wakati ambapo mantiki na fikira za watu si za kawaida, basi ubinadamu wao sio wa kawaida. Ikiwa, wakati huu, kazi ya Roho Mtakatifu iko ndani yako, basi Roho Mtakatifu atakuwa nawe pia kwa hakika. Lakini ikiwa Roho Mtakatifu yuko nawe, si lazima kwamba Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani yako, kwani Roho Mtakatifu hufanya kazi katika nyakati maalumu. Kuwa na uwepo wa Roho Mtakatifu kunaweza tu kudumisha kuishi kwa kawaida kwa watu, lakini Roho Mtakatifu hufanya kazi tu katika nyakati fulani. Kwa mfano, kama wewe ni kiongozi au mfanyakazi, unapofanya kazi ya unyunyizaji au kuruzuku kwa ajili ya kanisa, Roho Mtakatifu atakupa nuru kufikia maneno fulani ambayo ni ya kuwaadilisha wengine na yanayoweza kutatua baadhi ya matatizo ya utendaji ya kina ndugu—katika wakati kama huo, Roho Mtakatifu anafanya kazi. Wakati mwingine, unapokuwa ukila na kunywa maneno ya Mungu, Roho Mtakatifu hukupa nuru kwa maneno fulani ambayo yanahusiana na matukio uliyopitia hasa, yakikuruhusu upate ufahamu mkubwa zaidi wa hali zako; hii pia ni kazi ya Roho Mtakatifu. Wakati mwingine,

Ninapozungumza, ninyi husikiliza na huweza kupima hali zenu wenyewe dhidi ya maneno Yangu, na wakati mwingine ninyi huguswa au kutiwa moyo; hii yote ni kazi ya Roho Mtakatifu. Watu wengine husema kwamba Roho Mtakatifu anafanya kazi ndani yao nyakati zote. Hili haliwezekani. Ikiwa wangesema kwamba Roho Mtakatifu yuko nao kila mara, hilo lingekuwa la kweli. Ikiwa wangesema kwamba fikira na hisia zao ni za kawaida nyakati zote, hilo pia lingekuwa la kweli, na lingeonyesha kwamba Roho Mtakatifu yuko nao. Ikiwa wanasema kwamba Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani yao kila mara, kwamba wamepata nuru kutoka kwa Mungu na kuguswa na Roho Mtakatifu kila wakati, na wanapata ufahamu mpya kila wakati, basi hili si la kawaida hata kidogo! Ni la kupita uwezo wa binadamu kabisa! Bila tashwishi yoyote, watu kama hao ni pepo wabaya! Hata wakati ambapo Roho wa Mungu huja ndani ya mwili, kuna nyakati ambapo lazima Ale, na lazima apumzike—sembuse mwanadamu. Wale ambao wamemilikiwa na pepo wabaya huonekana kutokuwa na hisia na udhaifu wa mwili. Wanaweza kutelekeza na kuacha kila kitu, ni wasio na hisia, ni wenye uwezo wa kustahimili mateso na hawahisi uchovu hata kidogo sana, kana kwamba wamevuka mipaka ya mwili. Je, hili silo la kupita uwezo wa binadamu kabisa? Kazi ya pepo waovu ni ya kupita uwezo wa binadamu—hakuna mwanadamu anayeweza kutimiza mambo kama haya. Wale wasio na utambuzi huwa na wivu wanapowaona watu kama hao; Wao husema kwamba wana nguvu mno katika imani yao katika Mungu, wana imani kubwa na kamwe hawaonyeshi ishara yoyote ya udhaifu! Kwa kweli, hili lote ni dhihirisho la kazi ya pepo mwovu. Kwa sababu watu wa kawaida bila kuzuilika huwa na udhaifu wa binadamu; hii ni hali ya kawaida ya wale walio na uwepo wa Roho Mtakatifu.

Maana ya kusimama imara katika ushuhuda wa mtu ni ipi? Watu wengine husema kwamba wao hufuata tu jinsi wanavyofanya sasa na hawajishughulishi na kama wana uwezo wa kupata uzima; wao hawafuatilii uzima, lakini hawajiuzulu pia. Wanakubali tu kwamba hii hatua ya kazi hutekelezwa na Mungu. Je, huku si kushindwa katika ushuhuda wao? Watu kama hao hata hawashuhudii kuhusu kushindwa. Wale ambao wameshindwa hufuata haijalishi mengine yote na wanaweza kuufuatilia uzima. Wao hawaamini tu katika Mungu wa vitendo, lakini pia hujua kuifuata mipango yote ya Mungu. Hao ndio huwa na ushuhuda. Wale wasiokuwa na ushuhuda hawajawahi kuufuatilia uzima na bado wanafuata kwa kumaliza jambo kwa kubahatisha. Unaweza kufuata, lakini hili halimaanishi kwamba umeshindwa, kwani huna ufahamu wowote kuhusu kazi ya Mungu leo. Masharti fulani lazima yatimizwe ili kushindwa. Sio wote wanaofuata wameshindwa, kwani ndani ya moyo wako hufahamu chochote kuhusu kwa nini ni lazima umfuata Mungu wa leo, wala hujui vile ambavyo umefaulu hadi leo, nani amekusaidia mpaka leo. Utendaji wa imani katika Mungu wa watu wengine huwa wenye kuchanganyikiwa na kukanganyikiwa; hivyo, kufuata si lazima kumaanishe kwamba unakuwa na ushuhuda. Ushuhuda wa kweli ni nini hasa? Ushuhuda uliozungumziwa hapa una sehemu mbili: Mojawapo

ni ushuhuda wa kushindwa, na nyingine ni ushuhuda kwa kuweza kufanywa mkamilifu (ambako, kwa kawaida, utakuwa ushuhuda unaofuata majaribio makuu zaidi na majonzi ya siku za usoni). Kwa maneno mengine, ikiwa unaweza kusimama imara wakati wa majonzi na majaribio, basi utakuwa umekuwa na hatua ya pili ya ushuhuda. Kilicho cha maana sana leo ni hatua ya kwanza ya ushuhuda: kuweza kusimama imara wakati wa kila namna ya majaribu ya kuadibu na hukumu. Huu ni ushuhuda wa kushindwa. Hilo ni kwa sababu sasa ni wakati wa ushindi. (Unapaswa kujua kwamba sasa ni wakati wa kazi ya Mungu duniani; kazi kuu ya Mungu mwenye mwili duniani ni kushinda hili kundi la watu duniani wanaomfuata Yeye kupitia hukumu na kuadibu.) Kama una uwezo wa kushuhudia kuhusu kushindwa au la hakutegemei tu kama unaweza kufuata hadi mwisho, lakini, la muhimu zaidi, kama, unapopitia kila hatua ya kazi ya Mungu, unakuwa ba uwezo wa kuelewa kweli kuadibu na hukumu ya Mungu, na kama wewe kweli wewe unaitazama kazi hii yote. Hutaweza kupenyeza kwa kufuata tu hadi mwisho kabisa. Lazima uweze kusalimu amri kwa hiari wakati wa kila nafasi ya kuadibu na hukumu, lazima uwe na uwezo kuelewa kweli kila hatua ya kazi upitiayo, na lazima uweze kupata ufahamu wa, na utiifu kwa tabia ya Mungu. Huu ndio ushuhuda wa mwisho wa kushindwa ambao wewe unatakiwa kuwa nao. Ushuhuda wa kushindwa kimsingi unahusu ufahamu wako wa kupata mwili kwa Mungu. Cha msingi, hatua hii ya ushuhuda ni kwa kupata mwili kwa Mungu. Haijalishi kile ambacho unafanya au kusema mbele ya watu wa ulimwengu au wale wanaotawala; kilicho na maana kuliko vyote ni kama unaweza kuyatii maneno yote kutoka kinywani mwa Mungu na kazi Yake yote. Kwa hivyo, hatua hii ya ushuhuda inaelekezwa kwa Shetani na maadui wote wa Mungu—pepo na wenye uadui ambao hawaamini kwamba Mungu atakuwa mwili mara ya pili na kuja kufanya kazi hata kubwa zaidi, na zaidi ya hayo, hawaamini katika ukweli wa kurudi kwa Mungu kwa mwili. Kwa maneno mengine, inaelekezwa kwa wapinga Kristo wote—maadui wote wasioamini katika kupata mwili kwa Mungu.

Kumfikiria Mungu na kumtamani sana Mungu hakuthibitishi kwamba umeshindwa na Mungu; hili linategemea kama unaamini kwamba Yeye ni Neno lililopata mwili, kama unaamini kwamba Neno limepata mwili, na kama unaamini kwamba Roho amekuwa Neno, na Neno limeonekana katika mwili. Huu ndio ushuhuda muhimu. Haijalishi jinsi wewe unafuata, wala vile unavyojitumia mwenyewe; kilicho muhimu ni kama wewe unaweza kugundua kutoka kwa ubinadamu huu wa kawaida kwamba Neno limepata mwili na Roho wa kweli amepatikana katika mwili—kwamba ukweli wote, njia, na uzima umekuwa katika mwili, na Roho wa Mungu hakika amewasili duniani na Roho amekuwa katika mwili kwa kweli. Ingawa, kijuujuu, hili linaonekana kuwa tofauti na utungaji mimba kwa Roho Mtakatifu, katika kazi hii mnaweza kuona dhahiri zaidi kwamba Roho tayari amedhihirika katika mwili, na, zaidi ya hayo, kwamba Neno limepata mwili, na Neno limeonekana katika mwili. Unaweza kufahamu maana ya kweli

ya maneno haya: “Mwanzoni kulikuwa na Neno, na Neno alikuwa na Mungu, na Neno alikuwa Mungu.” Zaidi ya hayo, lazima ufahamu kwamba Neno la leo ni Mungu, na utazame Neno likiwa mwili. Huu ni ushuhuda bora zaidi unaoweza kuwa nao. Hili linathibitisha kwamba una ufahamu wa kweli wa Mungu kupata mwili—mbali na kumjua Yeye, lakini pia unajua kwamba njia unayoifuata leo ni njia ya uzima, na njia ya ukweli. Hatua ya kazi ambayo Yesu alitekeleza ilitimiza tu kiini cha “Neno alikuwako kwa Mungu”: Ukweli wa Mungu ulikuwako kwa Mungu, na Roho wa Mungu alikuwa na mwili na alikuwa asiyetenganishwa kutoka katika mwili huo. Yaani, mwili wa Mungu mwenye mwili ulikuwa na Roho wa Mungu, ambalo ni thibitisho kuu zaidi kwamba Yesu mwenye mwili alikuwa kupata mwili wa kwanza wa Mungu. Hatua hii ya kazi hasa inatimiza maana ya ndani ya “Neno lakuwa mwili,” ilichangia kwenye maana ya kina zaidi ya “naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu,” na inakuruhusu wewe uamini kwa uthabiti maneno “Hapo mwanzo kulikuwako na Neno.” Ambalo ni kusema, wakati wa uumbaji Mungu alikuwa na maneno, Maneno Yake yalikuwa na Yeye na yasiyotenganishwa kutoka Kwake, na katika enzi ya mwisho, Yeye anafanya nguvu na mamlaka ya maneno Yake yawe hata wazi zaidi, na kumruhusu mwanadamu kuziona njia Zake zote—kuyasikia maneno Yake yote. Hiyo ndiyo kazi ya enzi ya mwisho. Lazima uelewe mambo haya yote kabisa. Si suala la kuujua mwili, bali la jinsi unavyoelewa mwili na Neno. Huu ndio ushuhuda unaopaswa kuwa nao, kile ambacho kila mtu lazima akijue. Kwa sababu hii ni kazi ya kupata mwili kwa pili—na mara ya mwisho ambapo Mungu anapata mwili—inakamilisha kwa ukamilifu umuhimu wa kupata mwili, inatekeleza kabisa na kutoa kazi yote ya Mungu katika mwili, na kuitamatisha enzi ya Mungu kuwa katika mwili. Hivyo, lazima ujue maana ya kupata mwili. Haijalishi unavyokimbia huku na huko, au vile unavyotekeleza vizuri masuala mengine ya nje; kilicho muhimu ni kama unaweza kutii kwa kweli mbele ya Mungu mwenye mwili na kuitoa nafsi yako yote kwa Mungu, na kutii maneno yote yatokayo kinywani Mwake. Hili ndilo unalopaswa kufanya, na unalopaswa kutii.

Hatua ya mwisho ya ushuhuda ni ushuhuda wa kama unaweza kufanywa mkamilifu au la—ambako ni kusema, kwa kuwa umeelewa maneno yote yaliyonenwa na kinywa cha Mungu mwenye mwili, umekuja kupata ufahamu wa Mungu na kuwa na hakika kumhusu Yeye, unaishi kwa kudhihirisha maneno yote kutoka kinywani mwa Mungu, na kutimiza masharti ambayo Mungu anakwambia—mtindo wa Petro na imani ya Ayubu—kiasi kwamba unaweza kutii hadi kufa, kujitoa mwenyewe kabisa Kwake, na hatimaye kutimiza mfano wa mtu ambaye anafikia kiwango kilichowekwa, kinachomaanisha mfano wa mtu ambaye ameshindwa na kufanywa mkamilifu Baada ya kupitia hukumu na kuadibu kwa Mungu. Huu ndio ushuhuda wa mwisho—ni ushuhuda ambao mtu ambaye hatimaye amefanywa mkamilifu anapaswa kuwa nao. Hizi ni hatua mbili za ushuhuda mnaopaswa kuwa nao, na zinahusiana, kila moja ni ya msingi. Lakini

kuna jambo moja unalotakiwa kujua: Ushuhuda Ninaotaka kutoka kwako leo hauelekezwi kwa watu wa ulimwengu, wala kwa mtu yeyote mmoja, lakini kwa kile ambacho Nitakacho kutoka kwako. Kinatathminiwa na kama unaweza kuniridhisha Mimi, na kama unaweza kutimiza kabisa viwango vya masharti Yangu kwa kila mmoja wenu. Hili ndilo mnalopaswa kufahamu.

Utendaji (5)

Wakati wa Enzi ya Neema, Yesu alinena maneno fulani na Akatekeleza hatua moja ya kazi. Yote yalikuwa na muktadha, na yote yalikuwa ya kufaa kwa hali za watu wa wakati huo; Yesu alinena na kufanya kazi kama ilivyostahili muktadha wa wakati huo. Pia Alinena unabii kiasi. Alitabiri kwamba Roho wa ukweli angekuja katika siku za mwisho na angetekeleza hatua fulani ya kazi. Ambalo ni kusema, Hakuelewa chochote zaidi ya kazi ambayo Yeye Mwenyewe alipasa Afanye wakati wa enzi hiyo; kwa maneno mengine, kazi iliyoletwa na Mungu mwenye mwili ni yenye mipaka. Hivyo, Yeye hufanya tu kazi ya enzi ambayo Yeye yumo na Hafanyi kazi nyingine ambayo haihusiani na Yeye. Wakati huo, Yesu hakufanya kazi kulingana na hisia au maono, bali ilivyostahili wakati na muktadha. Hakuna aliyemwongoza au kumwelekeza Yeye. Kazi Yake nzima ilikuwa nafsi Yake—ilikuwa ni kazi iliyopaswa kutekelezwa na Roho wa Mungu mwenye mwili, ambayo ilikuwa kazi yote iliyokaribishwa na kupata mwili. Yesu alifanya kazi tu kulingana na kile ambacho Yeye Mwenyewe aliona na kusikia. Kwa maneno mengine, Roho alifanya kazi moja kwa moja; hakukuwa na haja ya wajumbe kumwonekana na kumpa ndoto, wala kwa nuru yoyote kubwa kumwagazia na kumkubalia Aone. Alifanya kazi kwa uhuru na bila vizuizi, ambayo ilikuwa kwa sababu kazi Yake haikutegemea hisia. Kwa maneno mengine, Alipofanya kazi, Hakutafuta kwa kupapasa na kubahatisha, lakini Alitimiza mambo kwa urahisi, Akifanya kazi na kunena kulingana na mawazo Yake mwenyewe na kile Alichooa kwa macho Yake mwenyewe, Akitoa riziki ya papo hapo kwa kila mwanafunzi aliyemfuata Yeye. Hii ndiyo tofauti kati ya kazi ya Mungu na kazi ya watu: Watu wanapofanya kazi, wao hutafuta na kupapasa huku na kule, kila mara wakiiga na kufikiria sana kwa kutegemea msingi uliowekwa na wengine ili kutimiza kuingia kwa ndani zaidi. Kazi ya Mungu ni utoaji wa kile Alichu, na Yeye hufanya kazi ambayo Yeye Mwenyewe anapaswa kufanya. Hatoi riziki kwa kanisa kwa kutumia ufahamu kutoka katika kazi ya mwanadamu yeyote. Badala yake, Yeye hufanya kazi ya sasa kwa kutegemea hali za watu. Hivyo, kufanya kazi kwa njia hii ni mara elfu huru zaidi kuliko kazi ambayo watu hufanya. Kwa watu, inaweza hata kuonekana kwamba Mungu hazingatii wajibu Wake na Hufanya kazi kwa namna yoyote Apendayo—lakini kazi yote ambayo Yeye hufanya ni mpya. Lakini, unapaswa kujua kwamba kazi ya Mungu mwenye mwili kamwe haitegemezwi kwa hisia. Wakati huo, baada ya Yesu kumaliza kazi Yake ya kusulubiwa, mara ambapo wanafunzi waliomfuata Yesu walikuwa wamefikia hatua fulani katika kupata kwao uzoefu, walihisi kwamba siku ya Mungu ilikuwa inakuja, na kwamba

wangekutana na Bwana hivi karibuni. Hiyo ilikuwa hisia waliyokuwa nayo, na kwao, hisia hii ilikuwa yenye umuhimu mkubwa kabisa. Lakini kwa kweli, hisia zilizo ndani ya watu si za kutegemewa. Walihisi kwamba labda walikuwa wanakaribia kufika mwisho wa njia, au kwamba yote waliyofanya na kuteseka kuliambiwa na Mungu. Vivyo hivyo, Paulo alisema kwamba alikuwa amemaliza mwendo wake, kwamba alikuwa amevipiga vita, na alikuwa amewekewa taji la haki. Hivyo ndivyo alivyohisi, na aliandika haya katika nyaraka na kuzituma kwa makanisa. Vitendo kama hivyo vilitokana na mzigo alioubeba kwa ajili ya makanisa, na hivyo vilipuuzwa na Roho Mtakatifu. Paulo aliposema maneno hayo, hakuwa na hisia ya mashaka, wala hakuhisi shutuma yoyote, na kwa hiyo aliamini kwamba mambo kama hayo yalikuwa ya kawaida sana na sahihi kabisa na kwamba yalikuwa yametoka kwa Roho Mtakatifu. Lakini yakitazamwa kutoka leo, haya hayakutoka kwa Roho Mtakatifu hata kidogo. Zilikuwa tu njozi za mwanadamu. Kuna njozi nyingi ndani ya wanadamu, na Mungu hazitilii maanani au kutoa maoni yoyote zinapotokea. Kazi nyingi ya Roho Mtakatifu haitekelezwi kupitia kwa hisia za watu—Roho Mtakatifu hafanyi kazi ndani ya hisia za watu kando na nyakati ngumu, za giza kabla ya Mungu kuwa mwili, au kipindi ambapo hakuna mitume au wafanyakazi. Wakati wa hatua hiyo, kazi ya Roho Mtakatifu huwapa watu hisia fulani maalumu. Kwa mfano: Wakati ambapo watu hawana mwongozo wa maneno ya Mungu, wanakuwa na hisia isiyoelezeka ya furaha wanapoomba; wanakuwa na hisia ya furaha mioyoni mwao, na wanakuwa na amani na utulivu. Mara wanapokuwa na mwongozo wa maneno, watu huhisi uchangamfu ndani ya roho zao, wana njia ya kutenda katika vitendo vyao na kwa kawaida pia wana hisia za amani na utulivu. Watu wanapokumbana na hatari, au Mungu anapowazuia kufanya mambo fulani, mioyoni mwao wanahisi kufadhaishwa na kutahayari. Hizi ni hisia anazopewa mwanadamu na Roho Mtakatifu kabisa. Hata hiyo, ikiwa mazingira mabaya yanaibua hali ya hofu, ikiwasababisha watu kuwa na wasiwasi mkuu na wenye uoga, huo ni udhihirisho wa kawaida wa ubinadamu na hauhusiani na kazi ya Roho Mtakatifu.

Watu kila mara huishi katikati ya hisia zao wenyewe, na wamefanya hivyo kwa miaka mingi sana. Wakiwa na amani mioyoni mwao, wao hutenda (wakiamini kwamba kuwa radhi kwao ni hisia ya amani), na wakati ambapo hawana amani ndani ya mioyo yao, wao hawatendi (wakiamini kutopenda au kutotaka kwao kuwa hisia ya wasiwasi). Mambo yakiendelea kwa urahisi, wao hudhani kwamba ni mapenzi ya Mungu. (Kwa kweli, ni jambo ambalo lilipaswa kufanyika kwa urahisi sana, hii ikiwa ndiyo sheria asili ya mambo.) Mambo yasipoenda kwa urahisi, wao hudhani kwamba siyo mapenzi ya Mungu. Wanapokumbana na kitu kisichoendelea kwa urahisi, wao hukoma. Hisia kama hizo si sahihi, na kutenda kulingana nazo kutasababisha kuchelewa kwingi. Kwa mfano, bila shaka kutakuwa na ugumu katika kuweka ukweli katika vitendo na hata zaidi katika kufanya mapenzi ya Mungu. Mambo mengi mazuri yatakuwa

magumu kutimiza. Jinsi tu msemu usemavyo, “Utambuzi wa mambo mazuri kawaida hutanguliwa na wakati mgumu.” Watu wana hisia nyingi sana katika maisha yao halisi, zikiwaacha wasijue cha kufanya kila mara na wasiwe na uhakika kuhusu mambo mengi. Hakuna kilicho dhahiri kwa watu wasipoweza kuelewa ukweli. Lakini kwa ujumla, wanapotenda ama kunena kulingana na hisia zao, mradi tu si jambo ambalo hukiuka kanuni za msingi, Roho Mtakatifu hajibu hata kidogo. Ni kama “taji la haki” aliyohisi Paulo: Kwa miaka mingi, hakuna yeyote aliyeamini kwamba hisia zake zilikuwa zenye makosa, wala Paulo mwenyewe hakuhihi kamwe kwamba hisia zake zilikuwa na makosa. Hisia za watu hutoka wapi? Hizo, bila shaka, ni mijibizo itokayo katika akili zao. Hisia tofauti husababishwa kulingana na mazingira tofauti, na mambo tofauti. Wakati mwingi, watu hufanya uamuzi kwa kutumia mantiki ya binadamu ambayo kupitia kwayo hupata seti ya fomula, jambo ambalo husababisha uundaji wa hisia nyingi za binadamu. Bila kujua, watu huingia katika uamuzi wao wenyewe wenye mantiki, na kwa njia hii, hisia hizi hugeuka kuwa kile ambacho watu hutegemea katika maisha yao; hizo huwa gongo la hisia katika maisha yao, kama vile taji la haki la Paulo” au “kukutana na Bwana hewani” kwa Witness Lee. Mungu takribani hana njia ya kuingilia katika hisia za mwanadamu, na lazima Azikubalie zikue kama zitakavyokua. Leo, Nimenena nawe wazi wazi kuhusu vipengele mbalimbali vya ukweli. Ukiendelea kufuata hisia zako, je, wewe bado huishi katika mambo yasiyo dhahiri? Wewe huyakubali maneno ambayo yameonyeshwa kwa dhahiri kwako, na kila mara wewe hutegemea hisia zako binafsi. Katika hili, je, wewe si kama kipofu anayegusa ndovu? Na ni nini ambacho utapata hatimaye?

Kazi yote inayofanywa na Mungu mwenye mwili leo ni halisi. Hiki si kitu ambacho unaweza kuhisi, au kitu unachoweza kufikiria, sembuse kuwa kitu ambacho unaweza kufahamu—ni kitu tu ambacho utaweza kuelewa wakati ambapo ukweli utadhihirika kwako. Wakati mwingine, hata yanapokujia, bado huwezi kuona kwa dhahiri, na watu hawataelewa hadi Mungu mwenyewe achukue hatua kuleta uwazi mkuu kwa mambo ya ukweli kuhusu kile kinachotokea. Wakati huo, kulikuwa na njozi nyingi miongoni mwa wanafunzi waliomfuata Yesu. Waliamini kwamba siku ya Mungu ilikuwa karibu kufika na wao wangekufa kwa ajili ya Bwana hivi karibuni na waweze kukutana na Bwana Yesu. Petro alingoja miaka saba mizima kwa sababu ya hisia hii—lakini bado haikufika. Walihisi kwamba maisha yao yalikuwa yamekomaa; hisia zilizokuwa ndani yao zilizidi mara dufu na hisia hizi zikawa kali zaidi, lakini walipitia kushindwa kwingi na hawakuweza kufanikiwa. Wao wenyewe hawakujua kilichokuwa kikiendelea. Je, kile ambacho kwa kweli kilitoka kwa Roho Mtakatifu hakingeweza kutimizwa? Hisia za watu si za kutegemewa. Hili sababu watu wana njia zao za kufikiria na mawazo yao wenyewe, wao hujenga ushirikiano mwingikutegemea muktadha na hali za wakati huo. Hasa, wakati ambapo jambo huwatendelea watu ambao njia za mawazo yao ni safi, wao huwa wenye

kusisimuka mno na hawawezi kujizuia kuunda ushirikiano mwingi. Hili hasa linahusisha “mabingwa” wenye maarifa na nadharia ya fahari sana, ambao uhusiano wao huwa hata mwingi zaidi baada ya miaka mingi ya kushughulika na ulimwengu; bila wao kujua, huo hutwaa mioyo yao na kugeuka kuwa hisia zao zenye nguvu kabisa, na wao huridhika nao. Watu wanapotaka kufanya jambo, hisia na mawazo yatatokea ndani yao na watadhani kwamba yako sahihi. Baadaye, wanapona kwamba hayajatimia, watu hawawezi kuelewa kilichoenda mrama. Labda wao huamini kwamba Mungu ameubadilisha mpango Wake.

Haizuiliki kwamba watu wote wana hisia. Wakati wa Enzi ya Sheria watu wengi pia walikuwa na hisia fulani, lakini makosa katika hisia zao yalikuwa machache zaidi kuliko ya watu wa leo. Hilo ni kwa sababu hapo awali, watu waliweza kutazama kuonekana kwa Yehova; wangeweza kuona wenye ujumbe na walikuwa na ndoto. Watu wa leo hawawezi kuona maono au wajumbe, na hivyo makosa katika hisia zao yamekua mara dufu. Wakati ambapo watu wa leo huhisi kwamba jambo fulani ni sahihi hasa na kwenda kulitia katika vitendo, Roho Mtakatifu hawashutumu na wana amani sana ndani yao. Baada ya ukweli huo, ni kupitia tu kwa ushirika au kusoma maneno ya Mungu ndipo wao hugundua walikuwa wamekosea. Kipengele kimoja cha hili ni kwamba hakuna wajumbe wanaonekana kwa watu, ndoto ni haba sana, na watu hawaoni chochote kuhusu maono angani. Kipengele kingine ni kwamba Roho Mtakatifu haongezi shutuma Zake na kufundisha nidhamu Kwake ndani ya watu; kuna kazi ya Roho Mtakatifu ndani yao kwa nadra sana. Hivyo, kama watu hawali na kunywa maneno ya Mungu, hawatafuti ukweli kwa njia ya vitendo, na hawaelewi njia ya kutenda, basi hawatavuna chochote. Kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu ni kama zifuatazo: Hazingatii kile ambacho hakihusu kazi Yake; ikiwa jambo haliko ndani ya mawanda ya mamlaka Yake, Yeye haingilii kati wala kuhisi kamwe, Akiwakubalia watu wasababishe matatizo yoyote wapendayo. Unaweza kutenda vyovyote utakavyo, lakini siku itakuja ambapo utajipata ukiwa mwenye kushikwa na wahaka na usijue la kufanya. Mungu hufanya kazi kwa lengo moja tu katika mwili Wake mwenyewe, Yeye haingilii kati kamwe katika kazi ya mwanadamu. Badala yake, Anajiepusha kabisa na ulimwengu wa mwanadamu, na Hufanya kazi ambayo Anapaswa kuifanya. Hutashutumiwa ukifanya kitu kibaya leo, wala hutatuzwa ukifanya kitu kizuri kesho. Haya ni mambo ya binadamu, na hayana uhusiano hata kidogo na kazi ya Roho Mtakatifu—hili haliko ndani ya mawanda ya kazi Yangu hata kidogo.

Katika wakati ambao Petro alikuwa akifanya kazi, alinena maneno mengi na kufanya kazi nyingi. Yawezekana kwamba hakuna kati ya kazi hiyo iliyotoka kwa mawazo ya binadamu? Kwa hiyo kuweza kutoka kabisa kwa Roho Mtakatifu haiwezekani. Petro alikuwa tu kiumbe wa Mungu, alikuwa mfuasi, alikuwa Petro, sio Yesu, na viini vyao havikuwa sawa. Ingawa Petro alitumwa na Roho Mtakatifu, si kila kitu alichofanya kilitoka kwa Roho Mtakatifu, kwani hata

hivyo, alikuwa mwanadamu. Paulo pia alinena maneno mengi na aliandika nyaraka zisizo chache kwa makanisa, ambazo baadhi yake zimekusanywa katika Biblia. Roho Mtakatifu hakuonyesha maoni yoyote, kwani huo ndio wakati ambao Paulo alikuwa akitumiwa na Roho Mtakatifu. Alipata uzoefu na maarifa fulani, na kuyaandika chini na kuyapisha kwa ndugu zake katika Bwana. Yesu hakuwa na mjibizo wowote. Kwa nini Roho Mtakatifu hakumkomesha wakati huo? Ilikuwa kwa sababu kuna baadhi ya uchafu unaoibuka kutoka katika namna ya kufikiri ya watu; hili haliepukiki. Aidha, vitendo vyake havikufikia kiwango cha kuwa ukatizaji au usumbufu. Wakati ambapo kuna kazi ya aina fulani kama hiyo ya ubinadamu, watu huona ikiwa rahisi zaidi kuikubali. Mradi uchafu wa namna ya kufikiri ya kawaida ya mwanadamu haujiingizi katika chochote, unachukuliwa kama kawaida. Kwa maneno mengine, watu wote wenye namna ya kufikiri ya kawaida wana uwezo wa kufikiria kwa njia hiyo. Wakati ambapo watu wanaishi katika mwili, wao huwa na namna yao wenyewe ya kufikiri, lakini hakuna njia ya kuondoa vitu hivi. Hata hivyo, baada ya kuipitia kazi ya Mungu kwa muda na kuelewa ukweli fulani, kutakuwa na namna hizi za kufikiri chache zaidi hizi ndani ya akili za watu. Wakati ambapo wamepitia mambo mengi, wataweza kuona kwa dhahiri na hivyo watapinga mambo kidogo zaidi. Kwa maneno mengine, wakati ambapo fikira za watu na uamuzi wenye mantiki hukanushwa, hisia zao zisizo za kawaida zitakuwa chache zaidi. Wale wote wanaoishi katika mwili huwanamna yao wenyewe ya kufikiri, lakini mwishowe, Mungu atawashughulikia hadi kwa kiwango ambapo namna yao wenyewe ya kufikiri hazitaweza kuwasumbua, hawatategemea tena hisia maishani mwao, kimo chao halisi kitakua, na watakuwa na uwezo wa kuishi kwa kufuata maneno ya Mungu ndani ya uhalisi, na hawatafanya tena mambo ambayo si dhahiri au yaliyo tupu, na kisha hawatafanya mambo mbayo yanasababisha usumbufu Kwa njia hii, njozi zao hazitakuwepo tena, na kuanzia wakati huu kuendelea mbele vitendo vyao vitakuwa kimo chao halisi.

Ukweli wa Ndani wa Kazi ya Ushindi (1)

Wanadamu kwa ajili ya kupotoshwa sana na Shetani, hawajui kuwa kuna Mungu na wameacha kumwabudu Mungu. Adamu na Hawa walipoumbwa mwanzoni, utukufu wa Yehova na Ushuhuda wa Yehova daima vilikuwepo. Lakini baada ya kupotoshwa, mwanadamu alipoteza utukufu na ushuhuda kwa sababu kila mtu alimwasi Mungu na kuacha kumcha kabisa. Kazi ya sasa ya kushinda ni kuupata ushuhuda na utukufu wote, na kuwafanya wanadamu wote wamwabudu Mungu, ili kuwepo na ushuhuda miongoni mwa viumbe wote. Hili ndilo linapaswa kufanywa katika hatua hii ya kazi. Wanadamu watashindwa vipi hasa? Watapata kushindwa kwa kutumia hii kazi ya maneno kumshawishi mwanadamu kwa dhati; kwa kutumia toba, hukumu, kuadibu, na laana isiyo na huruma dhibiti kabisa; na kwa kuweka wazi uasi wa mwanadamu na kwa kuhukumu upinzani wake ili ajue udhalimu wa mwanadamu na uchafu wake, mambo

ambayo yatatumiwa kuangazia tabia ya haki ya Mungu. Kwa kiwango kikubwa, ni matumizi ya maneno haya yatakayomshinda mwanadamu na kumshawishi kabisa. Maneno ndiyo njia ya kuwashinda wanadamu na wote wanaokubali ushindi lazima wakubali mapigo na hukumu ya maneno. Mchakato wa sasa wa kunena ni mchakato wa kushinda. Ni kwa njia gani watu wanapaswa hasa kushirikiana? Ni kwa kula na kunywa haya maneno ipasavyo na kuyafahamu. Watu hawawezi kujipatia ushindi wao wenyewe. Ni lazima, kwa kula na kunywa haya matamshi, upate kufahamu uovu na uchafu wako, uasi na udhalimu wako, na uanguke chini mbele ya Mungu. Ikiwa waweza kufahamu mapenzi ya Mungu kisha uyatie katika vitendo, na zaidi, uwe na maono, na ikiwa waweza kuyatii maneno haya kabisa na usitende kulingana na mapenzi yako, basi utakuwa umeshindwa. Na itakuwa ni haya maneno yamekuwezesha kushindwa. Ni kwa nini wanadamu walipoteza ushuhuda? Ni kwa sababu hakuna aliye na imani kwa Mungu au anamshikilia Mungu rohoni mwake. Kuwashinda wanadamu kunamaanisha watu wairudie hii imani. Watu daima wanauegemea ulimwengu, wakiwa na matumaini mengi sana, wakitaka kujua mengi sana kwa ajili ya maisha yao ya usoni, na wakiwa na mahitaji mengi ya kupita kiasi. Wanaifikiria na kuipangia miili yao kila mara wala hawatamani kutafuta njia ya kumwamini Mungu. Nyoyo zao zimetekwa na Shetani, wameacha kumheshimu Mungu, na wanatoa mioyo yao kwa Shetani. Ila mwanadamu aliumbwa na Mungu. Hivyo, mwanadamu amepoteza ushuhuda, kumaanisha amepoteza utukufu wa Mungu. Kusudi la kumshinda mwanadamu ni kuurejesha utukufu wa mwanadamu wa kumheshimu Mungu. Inaweza kusemwa hivi: Kuna watu wengi wasiofuatilia uzima; hata kama kuna wengine, idadi hiyo inaweza kuhesabiwa kwa vidole vya mtu. Watu wanahangaishwa sana kuhusu siku zao za baadaye na hawatilii maanani uzima kwa vyovyote vile. Watu wengine huasi dhidi ya Mungu na kumpinga, humhukumu bila Yeye kufahamu na hawatendi ukweli. Siwajali watu hawa kwa sasa, na Najizuia kushughulikia tabaka hili la wana wa uasi kwa sasa. Katika siku za usoni utaishi gizani, ukilia na kusaga meno yako. Wewe huhisi thamani ya nuru unapoishi ndani yake, lakini utatambua thamani yake mara tu unapoishi katika usiku wa giza. Utasikitika wakati huo. Unahisi sawa sasa, lakini itafika siku ambayo utasikitika. Siku hiyo itakapofika na giza lishuke na nuru isiweko tena, majuto yako yatakuwa yamechelewa. Ni kwa sababu bado huelewi kazi ya sasa ndio unakosa kutunza wakati wako sasa. Mara tu kazi ya ulimwengu mzima ianzapo, kumaanisha wakati ambapo kila kitu Nisemacho leo kimetimia, watu wengi watakuwa wakishikilia vichwa vyao kwa kilio cha uchungu. Je, huko sio kuingia katika giza na kulia na kusaga meno? Watu wote ambao hufuatilia uzima kweli na wamefanywa kuwa kamili watatumiwa, huku wana wote wa uasi ambao hawafai kutumiwa wataingia gizani, bila kupokea kazi yoyote ya Roho Mtakatifu kwa vyovyote vile na kubaki wasioweza kufahamu chochote. Hivyo wataingia katika adhabu kuomboleza na kutokwa na machozi. Kama umejiandaa vyema katika awamu hii ya kazi na maisha yako yamekomaa, basi wewe ni mtu unayefaa kutumiwa. Kama umejiandaa vibaya, basi hata kama umejitayarisha

kwa awamu inayofuata ya kazi utakuwa hufai. Wakati huo, hata kama utataka kujiandaa mwenyewe, nafasi itakuwa imepita. Mungu atakuwa ameondoka; utaenda wapi basi kutafuta aina ya nafasi iliyo mbele yako sasa, na utaenda wapi basi kupokea zoezi linalotolewa na Mungu binafsi? Wakati huo, haitakuwa Mungu akinena binafsi au akitoa sauti Yake. Utaweza tu kusoma kinachosemwa leo; utawezaje kuelewa kwa urahisi? Ni vipi ambavyo maisha ya baadaye yataweza kulingana na ya leo? Wakati huo, kulia na kusaga meno kwako hakutakuwa kupitia kifo kilicho hai? Baraka inatolewa kwako sasa lakini hujui namna ya kuifurahia; unaishi katika baraka, lakini hutambui hilo. Hili linaonyesha kwamba umeandikiwa mateso! Wakati huu watu wengine hupinga, wengine huasi, wengine hufanya hili au lile. Mimi hukupuuza tu; usifikiri kwamba Sizifahamu shughuli hizo zenu. Je, Sifahamu kiini chenu? Mbona muendeleo kwenda kinyume changu? Huamini katika Mungu ili ufuatilie uzima na baraka kwa ajili yako mwenyewe? Je, si kwa ajili yako mwenyewe ndio una imani? Sasa hivi Nafanya tu kazi ya kushinda na maneno Yangu. Mara tu kazi hii ya kushinda ikihitimishwa, mwisho wako utakuwa dhahiri. Je, Nahitaji kujieleza wazi zaidi?

Kazi ya sasa ya kushinda ni kazi inayokusudiwa kuweka wazi hatima ya mwanadamu itakuwaje. Ni kwa nini Ninasema kuwa kuadibu na hukumu ni hukumu mbele ya kiti cha enzi kikubwa cheupe cha siku za mwisho? Hulioni hili? Ni kwa nini kazi ya kushinda ni hatua ya mwisho? Je, si kudhihirisha kwa usahihi hatima ya kila tabaka la wanadamu? Si kumruhusu kila mtu, katika harakati ya kazi ya kushinda ya kuadibu na hukumu, kuonyesha tabia zake halisi na kisha kuwekwa katika aina yake baadaye? Badala ya kusema kuwa huku ni kuwashinda wanadamu, inaweza bora kusema kuwa huku ni kuonyesha hatima ya kila aina ya mwanadamu. Yaani, huku ni kuhukumu dhambi zao halafu kuonyesha matabaka mbalimbali ya wanadamu, na kwa njia hiyo kubaini kama ni waovu au ni wenye haki. Baada ya kazi ya kushinda, kazi ya kutuza mazuri na kuadhibu maovu inafuata: watu wanaotii kabisa, yaani walioshindwa kabisa, watawekwa katika hatua nyingine ya kusambaza kazi ulimwenguni kote; wasioshindwa watawekwa gizani na watapatwa na majanga. Hivyo, mwanadamu ataainishwa kulingana na aina yake, watenda maovu watawekwa pamoja na maovu, wasiwe na mwanga wa jua tena kamwe, na wenye haki watawekwa pamoja na mazuri, ili kupokea mwangaza na kuishi milele katika mwangaza. Mwisho wa vitu vyote uko karibu; mwisho wa mwanadamu umebainishwa wazi machoni mwake, na vitu vyote vitaainishwa kulingana na aina yake. Ni vipi basi wanadamu wataepuka kuathiriwa na kuanisha huku? Kufichua mwisho kwa kila jamii ya mwanadamu kutafanywa hatima ya kila kitu ikikaribia, na kutafanywa wakati wa kazi ya kushinda ulimwengu mzima (ikiwemo kazi yote ya kushinda kuanzia kazi ya sasa). Huku kufichua mwisho wa wanadamu kunafanywa mbele ya kiti cha hukumu, katika harakati ya kuadibu, na harakati ya kazi ya kushinda ya siku za mwisho. Kuwaainisha watu kwa kadri ya aina si kuwarudisha watu

katika matabaka yao ya asili. Hii ni kwa sababu binadamu alipoumbwa wakati wa uumbaji wa ulimwengu, kulikuwa tu na aina moja ya binadamu, kiume na wa kike. Hakukuwa na aina nyingi tofautitofauti. Ni baada tu ya miaka elfu kadhaa ya upotovu ndio matabaka mbalimbali ya binadamu yameibuka, mengine yakija chini ya miliki ya pepo wachafu, mengine chini ya miliki ya pepo waovu, na mengine, yanayofuatilia njia ya uzima, chini ya miliki ya Mwenyezi. Ni kwa njia hii tu ndio matabaka huibuka polepole miongoni mwa watu na ndio watu hujitenga katika matabaka ndani ya familia kubwa ya mwanadamu. Watu wote huja kuwa na “baba” tofauti; sio ukweli kwamba kila mtu yuko chini ya miliki ya Mwenyezi kabisa, kwa sababu uasi wa watu umezidi sana. Hukumu yenye haki hufichua nafsi ya kweli ya kila aina ya watu, bila kuacha chochote kikiwa kimefichika. Kila mtu huonyesha uso wake wa kweli katika nuru. Wakati huu, mwanadamu hayuko tena alivyokuwa mwanzoni na mfano wa asili wa mababu zake umepotea kitambo, kwa sababu vizazi visivyohesabika vya Adamu na Hawa vimenaswa na Shetani kwa muda mrefu, visijue tena jua la mbinguni, na kwa kuwa watu wamejazwa aina zote za sumu za Shetani. Hivyo, watu wana hatima zao za kufaa. Zaidi ya hayo, ni kwa msingi wa sumu zao zinazotofautiana ndio wanaainishwa kwa kadri ya aina, kumaanisha wanaainishwa kwa kiasi ambacho wanashindwa leo. Hatima ya mwanadamu si kitu kilichoamuliwa kabla tangu uumbaji wa dunia. Hii ni kwa sababu mwanzoni kulikuwa na jamii moja tu, ambayo kwa pamoja iliitwa “wanadamu,” na mwanadamu alikuwa bado hajapotoshwa na Shetani mwanzoni, na wanadamu wote waliishi katika mwangaza wa Mungu, bila giza kuwaandama. Lakini baada ya mwanadamu kupotoshwa na Shetani, kila jamii na aina ya watu walitapakaa ulimwenguni kote—kila jamii na aina ya watu waliotokana na ukoo mmoja ujulikanao kwa pamoja kama “wanadamu” uliojumuisha mwanamke na mwanamume. Wote walipotoshwa na mababu zao kutoka kwa nia za mababu zao wa kale sana—wanadamu waliojumuisha mwanamke na mwanamume (yaani, Adamu na Hawa wa asili, mababu zao wa kale sana). Wakati huo, watu wa pekee duniani walioongozwa na Yehova walikuwa Waisraeli. Watu wa aina mbalimbali walioibuka kutoka Israeli nzima (yaani kutoka ukoo wa asili) wakati ule walipoteza uongozi wa Yehova. Watu hawa wa mwanzo, wasiofahamu kabisa masuala ya ulimwengu wa wanadamu, walienda na mababu zao kuishi katika maeneo waliyodai kumiliki, mpaka wa leo. Hivyo hawatambui walipotoka vipi kutoka kwa Yehova na jinsi wamepotoshwa mpaka leo na aina yote ya pepo wachafu na roho waovu. Waliopotoshwa zaidi na kutiwa sumu mpaka leo hii, yaani ambao hatimaye hawawezi kukombolewa, hawatakuwa na budi ila tu kufuata mababu zao—pepo wachafu waliowapotosha. Wale wanaoweza kukombolewa hatimaye watakwenda hatima inayostahili wanadamu, yaani sehemu iliyotengwa kwa ajili ya waliokombolewa na walioshindwa. Kila kitu kitafanywa ili kukomboa wanaoweza kukombolewa, ila wale wasiosikia, watu wasioweza kutibika, chaguo lao pekee litakuwa kuwafuata mababu zao katika kuzimu ya kuadibu. Usidhani kuwa hatima yako iliamuliwa kabla tangu mwanzo na

imefichuliwa tu sasa. Ikiwa unadhani hivyo, basi, umesahau kuwa katika uumbaji wa mwanzo wa wanadamu, hakukuumbwa jamii tofauti ya Shetani? Je, umesahau kuwa ni aina moja tu ya mwanadamu, yaani Adamu na Hawa, ndiyo iliumbwa (ikiwa na maana kwamba ni mwanamume na mwanamke tu ndio waliumbwa)? Ungalikuwa uzao wa Shetani kutoka mwanzo, je, hilo halingemaanisha kuwa Yehova alipomuumba mwanadamu Alijumuisha jamii ya Shetani? Je, Angefanya jambo kama hilo? Alimuumba mwanadamu kwa ajili ya ushuhuda Wake; Alimuumba mwanadamu kwa ajili ya utukufu Wake. Angeumbaje kwa makusudi jamii ya vizazi vya Shetani ili kumuasi kwa makusudi? Je, Yehova angeweza kufanya hili? Ikiwa hivyo, ni nani angeweza kusema kuwa Yeye ni Mungu Mwenye haki? Nikisema sasa kuwa baadhi yenu mwishowe mtaenda na Shetani, haimaanishi kuwa ulikuwa na Shetani toka mwanzo; ila, inamaanisha umejishusha chini sana hivi kwamba japo Mungu amejaribu kukukomboa, bado umekosa kuupata ukombozi huo. Hakuna budi ila kukuweka katika jamii moja na Shetani. Hii ni kwa sababu huwezi kukombolewa, si kwa sababu Mungu si mwenye haki kwako, yaani, si kwa sababu Mungu kimakusudi alipangia majaliwa yako kama mfano halisi wa Shetani na baadaye kukuweka katika jamii moja na Shetani na kutaka uteseke kwa makusudi. Huo si ukweli wa ndani wa kazi ya kushinda. Ikiwa unaamini hilo, basi ufahamu wako unaegemea upande mmoja sana! Hatua ya mwisho ya kushinda ni ya kukomboa watu na vilevile kufichua mwisho wa kila mtu. Inaweka wazi upotevu wa watu kupitia hukumu na kwa njia hiyo kuwafanya watubu, waamke, na kufuatilia uzima na njia ya haki ya maisha ya mwanadamu. Ni ya kuamsha mioyo ya waliolala na wapumbavu na kuonyesha, kwa njia ya hukumu, uasi wao wa ndani. Hata hivyo, ikiwa watu bado hawawezi kutubu, bado hawawezi kufuata njia ya haki ya maisha ya mwanadamu na hawawezi kuutupa upotovu huu, basi watakuwa vyombo visivyoweza kukombolewa vya kumezwa na Shetani. Hii ndiyo maana ya kushinda—kuwakomboa watu na vilevile kuwaonyesha mwisho wao. Mwisho mzuri, mwisho mbaya—yote yanafichuliwa na kazi ya kushinda. Kama watu watakombolewa au kulaaniwa yote yanafichuliwa wakati wa kazi ya kushinda.

Siku za mwisho ni wakati ambao vitu vyote vitaainishwa kulingana na aina zake kupitia kushinda. Kushinda ni kazi ya siku za mwisho; kwa maneno mengine, kuhukumu dhambi za kila mtu ni kazi ya siku za mwisho. La sivyo, watu wangeainishwa vipi? Kazi ya kuainisha inayofanywa miongoni mwenu ni mwanzo wa kazi ya aina hiyo ulimwenguni kote. Baada ya hii, wale wa kila nchi na watu wote watapitia kazi ya ushindi. Hii inamaanisha kuwa watu wote wataainishwa kimakundi na kufika mbele ya kiti cha hukumu kuhukumiwa. Hakuna mtu na hakuna kitu kitakachoepuka kupitia huku kuadibu na hukumu, na hakuna mtu au kitu kinaweza kukwepa uainishaji huu; kila mtu atawekwa katika jamii. Hii ni kwa sababu mwisho u karibu kwa vitu vyote na mbingu zote na dunia zimefikia hatima yake. Mwanadamu anawezaje

kukwepa hatima ya maisha yake? Hivyo, mnaweza kuendelea na matendo yenu ya uasi kwa muda gani zaidi? Je, hamuoni kwamba siku zenu za mwisho ziko karibu sana? Ni vipi ambavyo wale wanaomcha Mungu na kutamani sana Aonekane watakosa kuona siku ya kuonekana kwa haki ya Mungu? Wanawezaje kukosa kupokea thawabu ya mwisho ya wema? Je, wewe ni yule atendaye mema, au yule atendaye maovu? Je, wewe ni yule akubaliye hukumu yenye haki na kisha kutii, au kisha hulaaniwa? Umekuwa ukiishi katika nuru mbele ya kiti cha hukumu, au katika giza jahanamu? Je, wewe mwenyewe si unayejua kwa dhahiri sana kama mwisho wako utakuwa wa thawabu au wa adhabu? Je, wewe si unayejua kwa dhahiri sana na kufahamu kwa kina sana kwamba Mungu ni mwenye haki? Kwa hiyo, kweli, mwenendo wako uko vipi na una moyo wako wa aina gani? Ninapoendelea kukushinda leo, unanihitaji Mimi kwa kweli kukueleza kinagaubaga kama mwenendo wako ni wa uovu au wa mema? Je, umeacha kiasi gani kwa ajili Yangu? Unaniabudu Mimi kwa kina gani? Wewe mwenyewe unajua kwa dhahiri sana ulivyo Kwangu—je, hiyo si kweli? Unapaswa kujua vizuri zaidi kuliko mtu yeyote jinsi utakavyokuwa hatimaye! Kweli Nakwambia, Niliwaumba tu wanadamu, na Nilikuumba wewe, lakini Sikuwakabidhi kwa Shetani; wala kuwafanya kwa makusudi muasi dhidi Yangu au kunipinga Mimi na kwa hivyo kuadhibiwa na Mimi. Hamjapata majanga haya kwa sababu mioyo yenu imekuwa migumu mno na mienendo yenu yenye kustahili dharau mno? Kwa hiyo si kweli kwamba mnaweza kuamua hatima yenu wenyewe? Je, si kweli kwamba mnajua ndani ya mioyo yenu, bora zaidi kuliko yeyote, vile mtaishia? Sababu ya Mimi kuwashinda watu ni kuwafichua, na pia kuhakikisha bora zaidi wokovu wako. Sio kukusababisha ufanye uovu au kwa makusudi kukusababisha uingie katika jahanamu ya uharibifu. Wakati utakapofika, mateso yako yote makuu, kulia kwako na kusaga meno—je, hayo yote hayatakuwa kwa ajili ya dhambi zako? Kwa hiyo, uzuri wako mwenyewe au uovu wako mwenyewe sio hukumu bora zaidi kukuhusu? Je, sio thibitisho bora zaidi ya kile ambacho mwisho wako utakuwa?

Leo, Ninafanya kazi miongoni mwa watu wateule wa Mungu walio Uchina kufichua tabia zao zote za uasi na kuufunua ubaya wao wote, na hili linatia muktadha wa kusema kila Ninachotaka kusema. Baadaye Nitafanya hatua nyingine ya kazi ya kuushinda ulimwengu wote. Nitatumia hukumu Yangu kwenu kuhukumu udhalimu wa kila mtu duniani kote kwa sababu ninyi watu ndio wawakilishi wa waasi miongoni mwa wanadamu. Wasiojikakamua watakuwa foili^[a] na vyombo vya kuhudumu tu, ila watakaojikakamua watatumika vizuri. Ni kwa nini Ninasema watakuwa foili? Ni kwa sababu maneno na kazi Yangu ya sasa vinalenga usuli wenu na kwa sababu mmekuwa wawakilishi na vielelezo vya uasi miongoni mwa wanadamu. Baadaye Nitapeleka maneno haya yanayowashinda kwa nchi za kigeni na kuyatumia kuwashinda watu wa huko, ila hutakuwa umeyafaidi. Je, hilo halitakufanya foili? Tabia potovu za wanadamu wote, matendo ya uasi wa mwanadamu, maumbile na sura mbaya za mwanadamu, zimeratibiwa zote

katika maneno yanayotumiwa kuwashinda nyinyi. Baadaye Nitayatumia maneno haya kuwashinda watu wa kila taifa na kila dhehebu kwa sababu nyinyi ni mfano, kigezo. Hata hivyo, Sikupanga kuwaacha kwa makusudi; ukikosa kufanya vizuri katika utafutaji wako na kwa hivyo unathibitisha kuwa asiyeponyeka, hautakuwa tu chombo cha huduma na foili? Wakati mmoja Nilisema kwamba hekima Yangu hutumiwa kutegemea njama za Shetani. Kwa nini Nilisema hilo? Je, huo si ukweli unaonga mkono Ninachosema na kufanya wakati huu? Kama huwezi kuchukua hatua, kama hujakamilishwa lakini badala yake unaadhibiwa, je, hutakuwa foili? Labda umeteseka sana katika wakati wako, lakini sasa bado huelewi chochote; hujui kila kitu kuhusu uzima. Ingawa umeadhibiwa na kuhukumiwa, hujabadilika kamwe na ndani yako kabisa hujapata uzima. Wakati wa kutathmini kazi yako utakapofika, utapitia majaribio makali kama moto na hata majonzi makuu zaidi. Moto huu utageuza nafsi yako yote kuwa majivu. Kama mtu asiye kuwa na uzima, mtu asiye na aushi ya dhahabu safi ndani yake, mtu ambaye bado amekatalia tabia potovu ya kale, na mtu asiyeweza hata kufanya kazi nzuri ya kuwa foili, ni jinsi gani hutaweza kuondoshwa? Je, mtu asiye na thamani yoyote, na asiye na uzima, anaweza kuwa na umuhimu wowote katika kazi ya ushindi? Wakati huo ufikapo, siku zenu zitakuwa ngumu zaidi kuliko za Nuhu na Sodoma! Maombi yenu hayatawasaidia wakati huo. Mara tu kazi ya wokovu ikiisha, utaanza tena kutubu? Mara tu kazi ya wokovu itakuwa imefanywa, hakutakuwa tena na kazi ya wokovu. Kitakachokuwepo ni mwanzo wa kazi ya kuadhibu uovu. Wewe hupinga, huasi, na hufanya mambo unayojua ni maovu. Je, wewe sio shabaha ya adhabu kali? Ninakuelezea hili wazi leo. Ukichagua kutosikia, wakati maafa yakufike baadaye, je, hautakuwa umechelewa kama utanza wakati huo tu kuhisi majuto na kuanza kuamini? Nakupa nafasi ya kutubu leo, lakini wewe hauko radhi kufanya hivyo. Unataka kungoja kwa muda gani? Mpaka siku ya kuadibu? Sikumbuki dhambi zako za zamani leo; Nakusamehe tena na tena, kugeuka kutoka upande wako mbaya kutazama tu upande wako mzuri, kwa sababu maneno na kazi Yangu yote ya sasa yanatakiwa kukuokoa wewe na sina nia mbaya kwako. Lakini unakataa kuingia; huwezi kutambua mema kutoka kwa mabaya na hujui namna ya kufurahia wema. Je, mtu wa aina hii hanui tu kungoja ile adhabu na malipo yenye haki?

Musa alipougonga mwamba, na maji yaliyokuwa yametolewa na Yehova yakaruka, ilikuwa ni kwa sababu ya imani yake. Daudi alipocheza kinubi kwa kunisifu Mimi, Yehova—moyo wake ukiwa umejaa furaha—ilikuwa ni kwa sababu ya imani yake. Ayubu alipowapoteza wanyama wake waliojaa kote milimani na mali nyingi sana, na mwili wake kujawa na majipu mabaya, ilikuwa ni kwa sababu ya imani yake. Alipoweza kusikia sauti Yangu, Yehova, na kuuona utukufu Wangu, Yehova, ilikuwa ni kwa sababu ya imani yake. Kwamba Petro aliweza kumfuata Yesu Kristo, ilikuwa ni kwa imani yake. Kwamba Alitundikwa misumari msalabani kwa ajili Yangu na kutoa ushahidi mtukufu, pia ilikuwa kwa imani yake. Yohana alipoona mfano

wa utukufu wa Mwana wa Adamu, ilikuwa kwa imani yake. Alipoona maono ya siku za mwisho, yote yalikuwa zaidi kwa sababu ya imani yake. Sababu ya yanayodaiwa kuwa mataifa mengi yasiyo ya Kiyahudi kupata ufunuo Wangu, na yakajua kwamba Nimerudi katika mwili kufanya kazi Yangu miongoni mwa wanadamu, pia ni kwa sababu ya imani yao. Wale wote wanaogongwa na maneno Yangu makali na bado wanatulizwa nayo na wanaookolewa—hawajafanya hivyo kwa sababu ya imani yao? Watu wamepokea vitu vingi sana kupitia imani. Kile ambacho wao hupokea sio baraka kila mara—kuhisi aina ya furaha na shangwe ambayo Daudi alihisi, au kuwa na maji yaliyotolewa na Yehova kama alivyofanya Musa. Kwa mfano, Ayubu alibarikiwa na Yehova kwa sababu ya imani yake, lakini pia alipitia maafa. Kama utapokea baraka au kupatwa na baa, yote ni matukio yaliyobarikiwa. Bila imani, hungeweza kupokea hii kazi ya kushinda, sembuse kuyaona matendo ya Yehova yanayoonyeshwa mbele ya macho yako leo. Hungeweza kuona, sembuse kuweza kupokea. Mabaa haya, maafa haya, na hukumu yote—kama haya hayangekufika, je, ungeweza kuona matendo ya Yehova leo? Leo hii ni imani inayokuruhusu kushindwa, na kushindwa ndiko kunakufanya uamini kila tendo la Yehova. Ni kwa sababu tu ya imani unapokea kuadibu na hukumu ya aina hii. Kupitia kuadibu na hukumu hizi, umeshindwa na kukamilishwa. Bila aina hii ya kuadibu na hukumu upokeayo leo hii, imani yako ingekuwa bure, kwa sababu humtambui Mungu; haijalishi unamwamini kiasi gani, imani yako bado itakuwa maonyesho matupu yasiyokuwa na misingi katika uhalisi. Ni baada tu ya kupokea aina hii ya kazi ya kushinda inayokufanya mtiifu kabisa ndipo imani yako inakuwa kweli na inayotegemewa na roho yako kumrudia Mungu. Japo umehukumiwa na kulaaniwa sana kwa sababu ya hili neno “imani,” una imani ya kweli, na unapokea kitu cha kweli zaidi, halisi zaidi, na chenye thamani zaidi. Hii ni kwa sababu ni katika harakati ya hukumu tu ndipo unaona hatima ya viumbe wa Mungu; ni katika hukumu hii ndio unapata kuona kuwa Muumba anapaswa kupendwa; ni katika kazi kama hiyo ya kushinda ndio unapata kuona mkono wa Mungu; ni katika kushinda huku unapata kutambua kwa ukamilifu maisha ya mwanadamu; ni katika kushinda huku unapata kujua njia ya haki ya maisha ya mwanadamu na kufahamu maana ya kweli ya “mwanadamu”; ni kupitia tu huku kushinda ndiko unaweza kuona tabia ya haki ya mwenye Uweza na uso Wake mzuri na mtukufu. Ni katika kazi hii ya kushinda ndiko unaweza kujifunza kuhusu asili ya mwanadamu na kufahamu “historia isiyokufa” ya mwanadamu; ni katika kushinda huku ndiko unapata kufahamu mababu za wanadamu na asili ya upotovu wa mwanadamu; ni katika kushinda huku ndio unapokea furaha na starehe pamoja na kuadibu, nidhamu, na maneno ya kuonya kutoka kwa Muumba kwa wanadamu ambao Aliwaumba; katika kazi hii ya kushinda, ndipo unapokea baraka na majanga ambayo mwanadamu anapaswa kupokea.... Je, haya yote si kwa ajili ya hiyo imani yako ndogo? Je, baada ya kuvipata vitu hivi vyote imani yako haijakua? Hujapata kiwango kikubwa ajabu? Hujasikia tu maneno ya Mungu na kuona hekima ya Mungu, lakini wewe binafsi umepitia pia

kila hatua ya kazi. Labda utasema kuwa usingekuwa na imani, basi usingepata aina hii ya kuadibu au aina hii ya hukumu. Ila unapaswa kufahamu kuwa bila imani, usingeweza tu kupokea aina hii ya kuadibu na ulinzi kutoka kwa mwenye Uweza, bali pia daima ungepoteza fursa ya kumwona Muumba. Usingejua asili ya wanadamu na kufahamu umuhimu wa maisha ya mwanadamu. Japo mwili wako utakufa na roho yako kuondoka, bado hutayafahamu matendo yote ya Muumba. Aidha hutafahamu kuwa Muumba alifanya kazi kubwa kiasi hicho duniani baada ya kuwaumba wanadamu. Kama mmojawapo wa hawa wanadamu Aliowaumba, je, uko tayari kutumbukia gizani kiasi hiki bila fahamu na kukumbana na adhabu ya milele? Ukijitenga na kuadibu na hukumu ya sasa, utapatana na kitu gani? Je, unafikiri ukishajitenga na hukumu ya sasa, utaweza kuepukana na haya maisha magumu? Je, si kweli kwamba ukiondoka “mahala hapa,” utakachokipata ni mateso machungu au majeraha kutoka kwa ibilisi? Je, waweza kukumbana na mchana na usiku zisizostahimilika? Je, unafikiri kwamba kwa kuepuka hukumu leo, unaweza kukwepa milele yale mateso ya siku zijazo? Ni kitu gani kitakukumba? Inaweza kuwa paradiso ya duniani unayoitarajia? Unafikiri unaweza kuepuka kuadibu kwa milele kwa baadaye kwa kuukimbia uhalisi kama ufanyavyo? Baada ya leo, je, utawahi kuweza kuipata fursa na baraka kama hii tena? Je, utapata fursa na baraka utakapokuwa umekumbwa na misukosuko? Je, utapata fursa na baraka wanadamu wote waingiapo katika pumziko? Maisha yako ya furaha ya sasa na hiyo familia yako ndogo yenye amani—vyaweza kuwa kibadala cha hatima yako? Iwapo una imani ya kweli, na iwapo unafaidi pakubwa kwa sababu ya imani yako, basi hayo yote ndiyo—wewe kiumbe—unapaswa kufaidi na vilevile kile ambacho ulipaswa kuwa nacho. Aina hii ya kushinda ndiyo ya faida zaidi kwa imani na maisha yako.

Kwa sasa unahitaji kufahamu kile anachotaka Mungu kwa wale wanaoshindwa, mtazamo Wake ni upi kwa wale wanaokamilishwa, na kile unachopaswa kuingia ndani mara moja. Mambo mengine unahitaji tu kuelewa kidogo. Mahubiri mengine kuhusu mafumbo huhitaji kujisumbua kuyaelewa. Si ya usaidizi sana kwa maisha, na inatosha tu kuyaangalia. Kwa mfano, mafumbo kama yale yanayohusu Adamu na Hawa unahitaji kuyaangalia. Kile ambacho Adamu na Hawa walikuwa wanalenga zama hizo, na kazi ambayo Mungu anataka kufanya leo Unahitaji kuelewa kwamba katika kushinda na kumkamilisha mwanadamu, Mungu anataka kumrudisha mwanadamu vile Adamu na Hawa walikuwa. Jinsi gani mtu lazima awe mkamilifu ili kufikia kiwango cha Mungu—unapaswa kufahamu vizuri hilo na kutaka kulifikia kabisa. Hilo linahusu utendaji wako na ni jambo unalopaswa kuelewa. Unahitaji tu kutafuta kuingia kwa kadri ya maneno yanayohusu mambo haya. Unaposoma kwamba “historia ya maendeleo ya wanadamu inarudi nyuma makumi ya maelfu ya miaka, unadadisi, na kwa hiyo unajaribu kuielewa pamoja na ndugu. “Mungu asema maendeleo ya wanadamu yanarudi nyuma miaka elfu sita, sawa? Ni nini hiki kuhusu makumi ya maelfu ya miaka?” Kuna maana gani ya kujaribu kuielewa hili?

Kama Mungu Mwenyewe amekuwa akifanya kazi kwa makumi ya maelfu ya miaka au mamia ya mamilioni ya miaka—je, Anakuhitaji uelewa hili? Hili si jambo ambalo wewe kama mtu aliyeumbwa anahitaji kujua kukihusu. Unaweza tu kuangalia aina hii ya mazungumzo; usijaribu kuyaelewa kama maono. Kile unachohitaji kujua kukihusu ni kile unachopaswa kuingia ndani na kupata uwazi sasa hivi. Tafakari na uelewe kuhusu haya. Ni wakati huo tu ndipo utapata kushindwa. Baada ya kusoma yaliyo hapo juu, kunapaswa kuwa na athari ya kawaida ndani yako: Mungu amejawa na hamu. Anataka kutushinda na kupata utukufu na ushuhuda. Tunapaswa kushirikiana vipi na Yeye? Lazima tufanye nini ili tuweze kushindwa kabisa na Yeye na kuwa ushuhuda Wake? Lazima tufanye nini kumwezesha Mungu kupata utukufu? Lazima tufanye nini ili kuturuhusu wenyewe kuishi chini ya miliki ya Mungu na si chini ya miliki ya Shetani? Hili ndilo watu wanapasa kufikiria kulihusu. Kila mmoja wenu anapaswa kuelewa umuhimu wa kushinda. Hilo ni jukumu lenu. Ni baada tu ya kupata uwazi huu ndio mtapata kuingia, mtajua hatua hii ya kazi, na mtakuwa watiifu kabisa. La sivyo, hamtatimiza utiifu wa kweli.

Tanbihi:

a. “Foili” Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Mbona Huna Hiari ya Kuwa Foili?

Wale ambao wanashindwa ni foili^[a], na ni baada tu ya kukamilishwa ndipo watu huwa vielelezo na mifano ya kazi ya siku za mwisho. Kabla ya kukamilishwa wao ni foili, vifaa, pamoja na vyombo vya huduma. Wale ambao wameshindwa kabisa na Mungu ndio dhihirisho la kazi Yake ya usimamizi, na vile vile mifano na vielelezo. Maneno haya ambayo nimetumia kuwaeleza watu kama hawa yanaweza kutokuwa ya kifahari, lakini yanafichua hadithi nyingi zenye kuvutia. Ninyi wenye imani ndogo mtabishana daima juu ya jina lisilokuwa lakifahari mpaka nyuso zenu zibadilike na kuwa nyekundu, na wakati mwingine hata mahusiano yanaharibika kama matokeo. Ingawa ni jina dogo tu, katika fikira zenu na katika imani yenu, hili si jina ambalo ni la umuhimu kabisa, bali ni jambo muhimu linalohusu majaliwa yenu. Basi, wale ambao hawana busara mara nyingi watapata hasara kubwa juu ya jambo dogo kama hili—huku ni kuokoa kidogo tu, na kisha kupoteza kingi. Kwa sababu tu ya jina lisilo na maana, mtatoroka na kamwe hamtarudi. Hii ni kwa sababu mnaona maisha kama hayana maana na mnaweka thamani kubwa sana juu ya majina mnayoitwa. Hivyo katika maisha yenu ya kiroho, na hata katika maisha yenu ya vitendo, mara nyingi mtakuza hadithi nyingi zilizo ngumu kueleweka na ambazo ni za ajabu kwa sababu ya dhana zenu kuhusu hadhi. Labda hamtakubali jambo hili, lakini Nitawaambia kwamba watu kama hawa kweli wapo katika maisha halisi, ingawa bado hamjafunuliwa mmoja mmoja. Mambo ya aina hii yamefanyika katika maisha ya kila mmoja wenu. Kama huamini hilo, tazama

tu nakshi iliyo chini kutoka kwa maisha ya dada (au ya kaka). Inawezekana kwamba mtu huyo kwa kweli ni wewe, au pengine ni mtu mnayefahamiana katika maisha yako. Kama Sikosei, nakshi hii inaelezea uzoefu ambao umekuwa nao. Hakuna kitu kinachokosa katika maelezo, hakuna fikira au wazo hata moja limeachwa nje, lakini yote yamerekodiwa kwa ukamilifu katika hadithi hii. Kama huamini jambo hilo, hebu isome tu kwanza.

Huu ni uzoefu mmoja mdogo kutoka kwa “mtu wa kiroho.”

Alihisi wasiwasi alipoona kwamba mambo mengi ambayo ndugu kanisani walifanya hayakuwa sambamba na mapenzi ya Mungu, hivyo alianza kuwakaripia, akisema: “Ninyi vitu viovu! Je, hamna dhamiri hata kidogo? Mbona mnafanya vitu visivyo vya busara? Mbona msiutafute ukweli badala ya kufanya chochote mpendacho? ... Ni ni nyinyi ndio ninaowaambia mambo haya, lakini wakati huo huo ni mimi mwenyewe ninayejichukia. Ninaona kwamba Mungu hawezi kuvumilia kabisa na ninahisi moto ndani yangu. Kweli niko tayari kutekeleza kazi ambayo Mungu ameaminia kwangu kwa ukamilifu na kweli ninataka niwatumikie. Ni kwamba tu sasa hivi mimi ni mnyonge sana. Mungu ametumia muda mwingi sana kwetu na Amenena maneno mengi sana, lakini bado tuko vivyo hivyo. Moyoni mwangu, daima nahisi kwamba bado nina deni kubwa sana....” (Alianza kulia, asiweze kuendelea kuzungumza.) Kisha, akaanza kuomba: “Ee Mungu! Nakuomba unipe nguvu na uniguse zaidi ya vile ambavyo Umefanya awali, na Roho Wako aweze kufanya kazi ndani yangu. Niko tayari kushirikiana na Wewe. Mradi hatimaye Upate utukufu, niko tayari sasa kujitolea Kwako kabisa, hata kama inamaanisha ni lazima nife. Tunataka kutoa sifa kubwa, ili ndugu zetu waweze kuimba na kucheza kwa furaha kulisifu jina Lako takatifu, kukutukuza, kukudhihirisha, kubaini kwamba kazi Yako ni ya kweli na kukujali Wewe kabisa kwa ajili ya mizigo Unayobeba....” Kwa ari aliomba kwa namna hii, na kweli Roho Mtakatifu alimpa mzigo. Kwa kipindi hiki, alibebeshwa mzigo sana, na alitumia siku nzima kusoma, kuandika, na kusikiliza. Alijishughulisha iwezekanavyo. Hali yake ya kiroho ilikuwa bora sana, na daima moyoni, alikuwa mwenye nguvu na wa kusumbuka. Mara kwa mara alidhoofika na kushindwa kuendelea, lakini kabla ya muda mrefu alirejesha tena hali yake ya kawaida. Baada ya kipindi cha muda kama huu, kuendelea kwake kulikuwa kwa kasi, aliweza kupata uelewa kiasi wa maneno mengi ya Mungu, naye pia alijifunza kwa wepesi nyimbo za kidini—kwa jumla, hali yake ya kiroho ilikuwa bora sana. Alipoona kwamba mambo mengi kanisani hayakukubaliana na mapenzi ya Mungu, alipata wasiwasi na kuwashutumu ndugu zake, akisema: “Je, huu ni upendo kwa jukumu lenu? Mbona hamwezi hata kulipa gharama ndogo kama hii? Kama hamtaki kulifanya, nitafanya....”

Alipokuwa akibeba mzigo, alihisi thabiti zaidi katika imani yake Roho Mtakatifu alivyofanya kazi zaidi. Mara kwa mara angekabiliwa na matatizo kiasi na kuwa hasi, lakini

aliweza kuyashinda haya. Yaani, alipopitia kazi ya Roho Mtakatifu, hata wakati hali yake ilikuwa nzuri sana, hangeweza kuepuka kukumbana na matatizo fulani au kudhoofika kwa namna fulani. Vitu kama hivyo hufanyika bila kuepukika, lakini kabla ya muda mrefu aliweza kutoka kwa hali hizo. Alipopitia udhaifu, angeomba na angehisi kwamba kimo chake mwenyewe kweli kilikuwa na upungufu, lakini alikuwa tayari kushirikiana na Mungu. Haidhuru kile Mungu alichofanya, alikuwa tayari kuridhisha mapenzi Yake na kutii mipango Yake yote. Kulikuwa na baadhi ya watu ambao walikuwa na maoni fulani na chuki bila sababu kwake, lakini aliweza kujiweka kando upande mmoja na kwa vitendo kushiriki katika ushirika nao. Hivi ndivyo hali za watu ziko wakati ambapo Roho Mtakatifu anatekeleza kazi Yake ya kawaida. Baada ya muda fulani, kazi ya Mungu ilianza kubadilika, na watu wote waliingia katika hatua nyingine ya kazi ambapo Mungu alikuwa na mahitaji tofauti kwao. Hivyo kulikuwa na maneno mapya yaliyonenwa yaliyoleta mahitaji mapya kwa watu: "... Nina chuki kwenu tu, kamwe si baraka. Sijawahi kuwa na fikira ya kuwabariki kamwe, wala Sijawahi kuwa na fikira ya kuwafanya kamili kwani ninyi ni waasi sana. Kwa sababu nyinyi si waaminifu na ni wadanganyifu, na kwa sababu mnakosa ubora wa tabia na nyinyi ni wa hadhi ya chini, kamwe hamjawahi kuwa karibu na macho Yangu au katika moyo Wangu. Kazi Yangu inafanywa kwa kusudi la kuwahukumu tu; mkono Wangu kamwe haujawahi kuwa mbali nanyi, wala kuadibu Kwangu. Nimeendelea kuwahukumu na kuwalaani. Kwa sababu hamna ufahamu Wangu, ghadhabu Yangu daima imekuwa juu yenu. Ingawa daima Nimefanya kazi miongoni mwenu, mnapaswa kujua mtazamo Wangu kuwaelekea. Si chochote ila maudhi—hakuna mtazamo au maoni mengine. Ninataka tu mtende kama foili kwa ajili ya hekima Yangu na uwezo Wangu mkubwa. Nyinyi si kitu zaidi ya foili Wangu kwa sababu haki Yangu inafichuliwa kupitia uasi wenu. Ninawataka mtende kama foili kwa ajili ya kazi Yangu, kuwa viambatisho vya kazi Yangu..." Mara tu alipoona maneno, "viambatisho" na "foili," alianza kufikiri: "Napaswa kufuataje kwa mujibu wa maneno haya? Baada ya kulipa gharama kama hiyo, mimi bado ni foili. Je, foili si mtendaji-huduma tu? Hapo zamani ilisemekana kwamba hatungekuwa watendaji huduma, kwamba tungekuwa watu wa Mungu, ilhali si bado sisi tuko hapo leo katika wajibwa wa watendaji huduma? Je, si watendaji huduma hawana uzima? Haijalishi navumilia mateso kiasi gani, Mungu hatanisifu kwa ajili ya jambo hili! Baada ya mimi kumaliza kuwa foili, mambo hayatakuwa yamekamilika? ..."

Alipofikiri zaidi kuhusu jambo hilo, ndivyo alivyokuwa mwenye huzuni zaidi. Alihisi hata vibaya zaidi alipokuja kanisani na kuona hali za ndugu zake: "Nyinyi hamko sawa! Mimi siko sawa! Nimekuwa hasi. Wai! Ni kipi kinaweza kufanywa? Mungu bado hatutaki. Katika kufanya kazi ya aina hii, hakuna namna hatatufanya hasi. Sijui ni nini kibaya na mimi. Sitaki hata kuomba. Hata hivyo, siko sawa sasa hivi na kweli sina nguvu ndani yangu. Nimeomba mara nyingi lakini bado siwezi, na siko tayari kuendelea. Hivi ndivyo ninavyoona jambo hili. Mungu anasema kwamba sisi ni foili, hivyo, je, si foili ni watendaji huduma tu? Mungu anasema

kwamba sisi ni foili, si wana Wake, na sisi si watu Wake, pia. Sisi si wana Wake, sembuse wana Wake wazaliwa wa kwanza. Sisi si chochote, bali ni foili tu. Kama hilo ndilo tulilo nalo, je, tunaweza kuwa na matokeo yenye kufaa? Foili hawana matumaini kwa sababu hawana maisha. Kama tungekuwa wana Wake, watu Wake, basi kungekuwa na matumaini katika jambo hilo—tungefanywa kamili. Je, foili wanaweza kuwa na uzima wa Mungu? Je, Mungu anaweza kuweka uhai ndani ya wale ambao hufanya huduma kwa ajili Yake? Wale Anaowapenda ni wale ambao wana uzima Wake, na wale tu walio na uzima Wake ni wana Wake, watu Wake. Ingawa mimi ni hasi na dhaifu, natumaini kwamba nyinyi nyote si hasi. Ninajua kwamba kuwa mwenye kusalia nyuma na kuwa hasi namna hii hakuwezi kuyaridhisha mapenzi ya Mungu, lakini siko tayari kuwa foili. Ninahofia kuwa foili. Vyovyote vile, nina nguvu kiasi fulani tu, na siwezi kuendelea sasa. Ninatumaini kwamba hakuna yeyote kati yenu atakayefanya jinsi nilivyofanya, lakini atapata kiasi fulani cha msukumo kutoka kwangu. Nahisi kwamba ni heri niende nife! Nitawaacha na maneno fulani ya mwisho kabla nikutane na mauti yangu—ninatumaini kwamba mnaweza kutenda kama foili hadi mwisho; labda hatimaye Mungu atawasifu foili....” Ndugu walipoona hili, walishangaa: “Ni jinsi gani anaweza kuwa hasi hivyo? Je, hajakuwa sawa kabisa katika siku kadhaa zilizopita? Mbona amepoteza ari yake ghafla? Je, mbona yeye si wa kawaida?” Alisema: “Usiseme mimi siwi kawaida. Kwa kweli, nina uhakika kuhusu kila kitu moyoni mwangu. Ninajua kwamba sijayaridhisha mapenzi ya Mungu, lakini, je, si hilo ni kwa sababu tu siko tayari kutenda kama foili Yake? Mimi sijafanya jambo lolote baya. Labda siku moja Mungu atabadili jina la ‘foili’ liwe ‘viumbe,’ na si hivyo tu, ila viumbe Wake ambao wanatumika naye kwa njia muhimu. Je, si kunayo matumaini kiasi katika jambo hili? Ninatumaini kwamba hamtakuwa hasi ama kuvunjika moyo, na mnaweza kuendelea kumfuata Mungu na kufanya kila muwezalo kutumika kama foili. Hata hivyo, siwezi kuendelea. Msiache matendo yangu yawawekee mipaka.” Watu wengine walisikia hayo, na wakasema, “Hata ukiacha kumfuata Yeye, tutaendelea, kwani Mungu hajawahi kututendea bila haki. Hatutazuiwa na uhasi wako.”

Baada ya kupitia tukio hili kwa kipindi cha muda, yeye bado alikuwa katika hali hasi juu ya kuwa foili, hivyo Nilimwambia: “Wewe huna ufahamu wa kazi Yangu. Huna ufahamu wa ukweli wa ndani, asili, au matokeo yaliyokusudiwa ya maneno Yangu. Hujui malengo ya kazi Yangu, wala hekima yake. Huna ufahamu wa mapenzi Yangu. Unajua tu kurudi nyuma kwa sababu wewe ni foili—unajishughulisha sana na hadhi! Wewe ni mpumbavu uliyeje! Hapo zamani Nimesema mengi sana kwako. Nimesema kuwa Nitakufanya mkamilifu; jje, umesahau? Je, sikuzungumza kuhusu kukamilishwa kabla ya kuzungumza kuhusu foili?” “Subiri, hebu nifikirie kulihusu. Ndiyo, hiyo ni sahihi! Ulisema mambo hayo kabla uliwahi kuzungumza kuhusu foili!” “Nilipozungumza kuhusu kukamilishwa, je, Sikusema kwamba ni baada tu ya

watu kushindwa ndiyo wangekamilishwa?” “Ndiyo!” “Je, maneno Yangu hayakuwa ya kweli? Je, hayakusemwa kwa nia njema?” “Ndiyo! Wewe ni Mungu ambaye hajawahi kusema kitu chochote cha udanganyifu—hakuna yeyote anayeweza kuthubutu kukana jambo hili. Lakini mnazungumza kwa njia nyingi sana tofauti.” “Je, njia Zangu za kuzungumza hazibadiliki kulingana na hatua tofauti za kazi? Je, maneno Ninayoyasema hayafanywi na kusemwa kulingana na mahitaji yako?” “Wewe hufanya kazi kulingana na mahitaji ya watu na Wewe huwapa kile wanachohitaji. Jambo hili si la uwongo!” “Je, basi mambo ambayo Nimekwambia hayajakuwa yenye manufaa? Je, kuadibu Kwangu hakujatekelezwa kwa ajili yako?” “Je, bado unawezaje kusema kwamba ni kwa ajili yangu mwenyewe! Umeniadibu hadi karibu nife—sitaki kuishi zaidi. Leo Unasema hili, kesho Unasema lile. Ninajua kwamba Wewe kunikamilisha ni kwa ajili yangu mwenyewe, lakini hujanikamilisha—Wewe unanifanya foili na bado unaniadibu. Unanichukia, sivyo? Hakuna yeyote anayethubutu kuamini maneno Yako, na ni sasa tu Nimeona dhahiri kwamba kuadibu Kwako ni ili kutatua tu chuki iliyo katika moyo Wako, si ili kuniokoa. Awali ulinificha ukweli; Ulisema ungenikamilisha na kwamba kuadibu kulikuwa kwa ajili ya kunikamilisha. Hivyo daima nimetii kuadibu Kwako; sikuwahi kufikiri kwamba leo ningebeba jina la foili. Mungu, je, haingekuwa bora zaidi kama Ugenitaka nitende kama kitu kingine chochote? Ni lazima unishurutishe kufanya wajibu wa foili? Hata ninaweza kukubali kuwa bawabu katika ufalme. Nimekuwa nikikimbia huku na kule nikijitumia, lakini mwishowe mikono yangu ni mitupu—sina chochote kabisa. Ihali hata sasa Unaniambia Utanifanya nitende kama foili Yako. Ninawezaje hata kuonyesha uso wangu?” “Ulikuwa unazungumza kuhusu nini? Nimefanya kazi nyingi mno ya kuadibu zamani, na wewe huielewi? Je, wewe unajifahamu mwenyewe kwa kweli? Je, jina la ‘foili’ pia si hukumu ya maneno? Je, unafikiri kwamba kuzungumza Kwangu kuhusu foili pia ni njia, namna ya kukuhukumu? Basi utanifuataje?” “Bado sijapanga jinsi ya kukufuata Wewe. Kwanza ninataka kujua: Je, mimi ni foili au la? Je, foili pia wanaweza kukamilishwa? Je, jina la ‘foili’ linaweza kubadilishwa? Ninaweza kutoa ushuhuda mkubwa sana kupitia kuwa foili, na kisha kuwa mtu ambaye amekamilishwa, ambaye ni mfano wa kumpenda Mungu, na mwandani wa Mungu? Ninaweza kukamilishwa? Niambie ukweli!” “Je, huna habari kwamba daima vitu vinakua, daima vinabadilika? Mradi sasa hivi uko tayari kuwa mtiifu katika kazi yako kama foili basi utaweza kubadilika. Kama wewe ni foili au la haina uhusiano wowote na hatima yako. Cha muhimu ni kama unaweza kuwa mtu ambaye ana badiliko katika tabia ya maisha yake au la.” “Je, unaweza kuniambia iwapo unaweza kunikamilisha au la?” “Mradi ufuata na kutii mpaka mwisho, Ninakuhakikishia kwamba Ninaweza kukufanya kamili.” “Na itanibidi nipitie mateso ya aina gani?” “Utapitia shida, na vile vile hukumu na kuadibu kwa maneno, hasa kuadibu kwa maneno, ambako ni sawa na kuadibiwa kwa kuwa foili!” “Kuadibu sawa na ya foili pia? Hivyo, kama ninaweza kukamilishwa na Wewe kwa kupitia shida, kama kuna matumaini, basi hiyo ni sawa. Hata kama ni chembe ya matumaini

tu, ni bora zaidi kuliko kuwa foili. Jina hilo, ‘foili,’ husikika kuwa baya sana. Siko tayari kuwa foili!” “Ni nini kibaya sana kuhusu foili? Je, si foili ni wazuri kikamilifu kwa njia yao wenyewe? Je, foili hawastahili kufurahia baraka? Nikisema kwamba foili wanaweza kufurahia baraka, basi utaweza kufurahia baraka. Si ukweli kwamba majina ya watu hubadilika kwa sababu ya kazi Yangu? Na ilhali jina tu linakusumbua kiasi hiki? Ukweli kwamba wewe ni foili wa aina hii kunastahili kabisa. Je, uko tayari kufuata au la?” “Kwa hivyo, unaweza kunifanya kamili au la? Je, Unaweza kuniruhusu nifurahie baraka Zako?” “Je, uko tayari kufuata mpaka mwisho au la? Je, uko tayari kujitoa?” “Acha nilifikirie. Foili pia anaweza kufurahia baraka Zako, na anaweza kukamilishwa. Baada ya kufanywa mkamilifu nitakuwa mwandani Wako na kufahamu mapenzi Yako kwa ukamilifu, na nitamiliki Unachomiliki. Nitaweza kufurahia kile Unachofurahia, na nitajua kile Unachojua. ... Baada ya kupitia shida na kukamilishwa, nitaweza kufurahia baraka. Hivyo ni baraka zipi Nitakazofurahia kwa kweli?” “Usiwe na wasiwasi juu ya baraka utakazofurahia. Hata Ngingekwambia, mambo haya yanazidi mawazo yako. Baada ya kuwa foili mzuri, utashindwa, na utakuwa foili mwenye mafanikio. Huu ni mfano na kielelezo cha mtu ambaye ameshindwa, lakini bila shaka unaweza tu kuwa mfano na kielelezo baada ya kushindwa.” “Mfano na kielelezo ni nini?” “Ni mfano na kielelezo kwa wote wasio Wayahudi, yaani, wale ambao hawajashindwa.” “Hilo linawajumuisha watu wangapi?” “Ni watu wengi sana. Si tu watu wale elfu nne au tano kati yenu—wale wote ambao wanalikubali jina hili katika dunia nzima lazima washindwe.” “Hivyo si miji mitano au kumi tu!” “Usiwe na wasiwasi kuhusu hili sasa, na usijishughuliche kupita kiasi. Lenga tu jinsi unavyopaswa kupata kuingia sasa hivi! Ninakuahidi kwamba unaweza kukamilishwa.” “Hadi kiwango kipi? Na ni baraka zipi ninazoweza kufurahia?” “Kwa nini una wasiwasi sana? Nimeahidi kwamba unaweza kufanywa mkamilifu. Je, umesahau kwamba Mimi ni mwaminifu?” “Ni kweli kwamba Wewe ni mwaminifu, lakini baadhi ya mbinu Zako za kuzungumza daima zinabadilika. Leo Unasema Unaahidi kwamba ninaweza kukamilishwa, lakini kesho unaweza kusema hakuna uhakika. Na kwa watu wengine unasema ‘Ninaahidi kwamba mtu kama wewe hawezi kukamilishwa.’ Sijui kile kinachoendelea na maneno Yako. Hasa sithubutu kuliadini kwa urahisi.” “Hivyo unaweza kujitoa au la?” “Kutoa nini?” “Kutoa maisha yako ya baadaye na matumaini yako.” “Ni rahisi kuyaachilia mambo hayo! Jambo kuu ni jina la ‘foili’—kwa kweli silitaki. Ukiondoa jina hilo kutoka kutoka kwangu basi nitakaribisha chochote, nitaweza kufanya chochote. Je, haya si mambo madogo tu? Je, Unaweza kuondoa jina hilo?” “Hilo litakuwa jambo rahisi tu, sivyo? Kama Ninaweza kukupa jina hilo, bila shaka pia Ninaweza kuliondoa. Lakini sasa si wakati wa hilo. Lazima kwanza ukamilishe uzoefu wako wa hatua hii ya kazi, na ni hapo tu ndipo unaweza kupata jina jipya. Zaidi mtu alivyo kama wewe, ndivyo anahitaji zaidi kuwa foili. Unavyoogopa zaidi juu ya kuwa foili, ndivyo Nitakavyokupachika jina hilo zaidi. Mtu kama wewe lazima apewe nidhamu kali na kushughulikiwa. Kadiri mtu alivyo muasi, ndivyo atakavyokuwa

mtendaji huduma zaidi, na mwishowe, hatapata chochote.” “Kuona kwamba natafuta kwa bidii sana, kwa nini nisiweze kulitupilia mbali jina la ‘foili’? Tumekufuata hii miaka yote na kuteseka sana. Tumekufanyia mambo mengi. Tumepita katika upepo na mvua; tunakaribia mwisho wa ujana wetu. Hatujaoa wala kuanzisha familia, na wale kati yetu ambao wamefanya hivyo bado wamejitokeza wazi. Nilikuwa shuleni wakati wote hadi katika shule ya upili, lakini mara tu niliposikia kwamba ulikuwa Umekuja, niliacha nafasi yangu ya kwenda chuo kikuu. Na Unasema kwamba sisi ni foili! Tumepoteza mengi mno! Tunafanya mambo haya yote, lakini sasa inatokea kwamba sisi ni foili Zako tu. Je, jambo hili linawafanya wenzangu tuliosoma nao darasani na marika wangu kunifikiria mimi nini? Wanaponiona na kuuliza juu ya cheo changu na hadhi yangu, ninakosaje kuwa na aibu kuwaambia? Mwanzoni, nililipa gharama yoyote kwa sababu ya imani yangu Kwako na wengine wote walinidhihaki kama mpumbavu. Lakini bado nilifuata na nilikuwa na hamu ya wakati ambapo siku yangu ingekuja, na ambapo ningewaonyesha wale wote ambao hawakuamini. Lakini badala yake, leo Unaniambia kwamba mimi ni foili. Kama Ungenipa jina la chini kabisa, kama Ungeniruhusu niwe mmoja wa watu wa ufalme, hilo lingekuwa sawa! Hata kama singekuwa mwanafunzi Wako au msiri Wako, ningekuwa sawa tu kuwa mfuasi Wako! Tumekufuata miaka hii yote, tumeziacha familia zetu, na imekuwa vigumu sana kuendelea kutafuta muda huo wote mpaka sasa, na kile tulicho nacho ni jina la ‘foili’ tu! Nimeacha kila kitu kwa ajili Yako; Nimeacha utajiri wote wa dunia hii. Kabla, mtu fulani alinitambulisha kwa mtu ambaye angeweza kuwa mwenzi. Kwa kweli alikuwa mwenye sura nzuri na alivalia vizuri, alikuwa mwana wa kiongozi wa serikali wa ngazi ya juu. Wakati huo nilivutiwa naye. Lakini mara tu niliposikia kwamba Mungu alikuwa ameonekana na alikuwa akitekeleza kazi Yake, kwamba Ulikuwa Utuongoze kuingia katika ufalme na kutukamilisha, na kwamba Ulikuwa umetuomba tuwe na uamuzi wa kutosita katika kuwacha kila kitu nyuma, niliposikia hayo, niliona kwamba sikuwa na uamuzi wowote hata kidogo. Kisha nilijikaza kisabuni na kukataa fursa hiyo. Baada ya hapo, alituma zawadi kwa familia yangu mara kadhaa, lakini hata sikuziangalia. Je, Unafikiri kwamba nilikuwa nimekasirika wakati huo? Kilikuwa kitu kuziri sana lakinihakikufanikiwa. Ningekosaje kufadhaika? Nilifadhaika kukihusu kwa siku kadhaa hivi kwamba singeweza kulala usiku, lakini hatimaye bado nilikiacha. Kila wakati nilipoomba, nilisisimuliwa na Roho Mtakatifu, ambaye Alisema: ‘Je, uko tayari kutoa kila kitu kwa ajili Yangu? Je, uko tayari kujitumia kwa ajili Yangu?’ Kila Nilipofikiri juu ya maneno hayo Yako ningelia. Niliguswa na nikalia kwa huzuni mara nyingi zaidi ya ninavyojua. Mwaka mmoja baadaye nilisikia kwamba mtu huyo alikuwa ameo. Ni wazi kwamba, nilikuwa mwenye taabu sana, lakini bado niliacha jambo hilo kwa ajili Yako. Haya yote licha ya kutaja kuwa chakula changu na mavazi ni duni—niliacha ndoa hiyo, niliyaacha haya yote, kwa hivyo Hupaswi kunitaka nitende kama foili! Niliacha ndoa yangu, tukio muhimu zaidi maishanimwangu, kwa ajili tu ya kujidhabihu Kwako. Maisha yote ya mtu si kitu chochote zaidi

ya kupata mwenzi mzuri na kuwa na familia yenye furaha. Niliacha hili, hili bora kati ya mambo yote, na sasa sina chochote na mimi niko mpweke. Ni wapi Ungenitaka niende? Nimeteseka tangu nilipoanza kukufuata. Sijakuwa na maisha mazuri. Nimeiacha familia yangu na amali yangu pamoja na furaha za mwili, na dhabihu hii ambayo sote tumetoa bado haitoshi kufurahia baraka Zako? Hivyo sasa ni suala hili la ‘foili’. Mungu, kwa kweli Wewe umezidi! Tuangalie—hatuna kitu chochote cha kutegemea katika dunia hii. Wengine wetu tumewaacha watoto wetu, wengine tumeacha kazi zetu, wenzi wetu,^[b] na kadhalika; tumeacha furaha zote za mwili. Kuna tumaini lipi lingine kwetu? Tunawezaje kuendelea kuishi katika ulimwengu? Je, kujitoa huku ambako tumejitoa hakuna thamani ya peni moja? Huwezi kuona hilo kabisa? Hadhi yetu ni duni na ubora wetu wa tabia ni pungufu—tunakubali jambo hili, lakini wakati upi hatujawahi kutii kile Ulichotaka tufanye? Sasa unatuacha bila huruma na ‘kutulipa’ kwa jina ‘foili’? Je, kujitolea kwetu kumetuletea hili tu? Hatimaye, watu wakiniuliza ni nini nimepata kutokana na kumwamini Mungu, je, kweli naweza kuwaruhusu waone neno hili ‘foili’? Ninawezaje kufungua mdomo wangu kusema kwamba mimi ni foili? Siwezi kueleza hilo kwa wazazi wangu, na siwezi kulieleza kwa yule angeweza kuwa mwenzi wangu wa zamani. Nimelipa gharama kubwa sana, na kile ninachopata kama malipo ni kuwa foili! Aa! Nahisi huzuni sana!” (Alianza kuyapiga mapaja yake na kulia.) “Ningesema kwamba sasa kwa kuwa sasa Sikuwa nikupe jina la foili lakini badala yake Ningeufanya mmoja wa watu Wangu na Nikuamuru uende na ukaeneze injili, kama Ningeкупа hadhi ya wewe kufanya kazi, je, ungeweza kuifanya? Kwa kweli ni kipi ambacho umepata kutokana na hatua baada ya hatua ya kazi hii? Ilhali uko hapa ukiburudisha Mimi na hadithi yako—huna aibu! Unasema kwamba umelipa gharama lakini hujapata chochote. Inawezekana kwamba Nimepuuza kukwambia masharti Yangu ni gani ya kumpata mtu? Kazi Yangu ni kwa ajili ya nani? Je, unajua? Uko hapa ukirudisha manung’uniko ya zamani! Je, hata unahesabika kama mwanadamu tena? Je, huchukui kuteseka kokote kwamba ulipitia kwa hiari yako mwenyewe? Na, je, kuteseka kwako hakukuwa ili kupata baraka? Je, umetosheleza mahitaji Yangu? Yote unayotaka ni kupata baraka. Huna aibu! Ni lini mahitaji Yangu kwako yaliwahi kuwa ya lazima? Ikiwa uko tayari kunifuata ni lazima unitii katika mambo yote. Usijaribu kujadili juu ya masharti. Hata hivyo, Nilikuambia awali kuwa njia hii ni njia ya kuteseka. Imejawa na uwezekano wa kutia hofu, na msaada kidogo. Je, umesahau? Nimesema jambo hili mara nyingi. Ikiwa uko tayari kuteseka basi Nifuate. Kama huko tayari kuteseka, basi acha. Sikulazimishi—uko huru kuja au kwenda! Hata hivyo, hivi ndivyo kazi Yangu inavyofanywa, na Siwezi kuchelewesha kazi Yangu yote kwa sababu ya uasi wako binafsi. Unaweza kuwa huko tayari kutii, lakini kuna wengine ambao wako tayari. Nyinyi nyote ni watu walio tayari kufanya lolote! Huogopi chochote! Unajadili nami juu ya masharti—unataka kuendelea kuishi au la? Unajipangia mwenyewe na kupigania umaarufu na faida yako mwenyewe. Je, kazi Yangu yote si kwa ajili yenu? Je, wewe ni kipofu? Kabla Nipate mwili,

hungeweza kuniona, na maneno haya ambayo umeongea yangesameheka wakati huo, lakini sasa Mimi Nimepata mwili na Ninafanya kazi kati yenu, lakini bado huwezi kuona? Ni nini usichoelewa? Unasema umepata hasara; hivyo Nimekuwa mwili ili kuwaokoa nyinyi watu waliokata tamaa na Nimefanya kazi kubwa sana, na hata sasa bado mnalalamika—hamwezi kusema kwamba Nimepata hasara? Je, si kile ambacho Nimefanya ni kwa ajili yenu kabisa? Ninawapa watu jina hili kulingana na kimo chao cha wakati uliopo. Nikiwaita ‘foili,’ basi unakuwa foili mara moja. Vivyo hivyo, Nikikuita ‘mmoja wa watu wa Mungu,’ basi hilo ndilo unalokuwa mara moja. Chochote Nikuitacho, hicho ndicho ulicho. Je, si yote yanatimizwa kwa maneno machache kutoka kwa kinywa Changu? Na haya maneno Yangu machache yanakughadhibisha sana? Sawa basi, Niwie radhi! Usipotii sasa, hatimaye utalaaniwa—utafurahi wakati huo? Huzingatii njia ya maisha lakini unalenga tu hadhi na jina lako; je, maisha yako yakoje? Sikani kwamba umelipa gharama kubwa, lakini angalia kimo na matendo yako mwenyewe—na hata sasa, bado unajaribu kujadili masharti. Je, hiki ni kimo ambacho umekipata kupitia katika uamuzi wako? Je, bado una uadilifu wowote? Je, una dhamiri? Je, ni Mimi niliyefanya kitu kibaya? Je, mahitaji Yangu kwako yalikuwa ya makosa? Haya, ni nini? Ningetaka utende kama foili kwa siku chache na bado huko tayari kufanya hivyo. Huo ni uamuzi wa aina gani? Nyinyi nyote ni wenye mioyo dhaifu, nyinyi ni waoga! Kuwaadhibu watu kama nyinyi sasa ni jambo la linalotarajiwa!” Mara tu Niliposema jambo hili, hakusema neno lolote.

Kupitia kazi ya aina hii sasa, lazima muwe na ufahamu fulani kuhusu hatua za kazi ya Mungu na mbinu Zake za kuwabadili watu. Kuwa na hili ndiyo njia ya pekee ya kutimiza matokeo katika mabadiliko. Katika kutafuta kwenu, mna dhana, matumaini, na siku za baadaye nyingi sana za kibinafsi. Kazi ya sasa ni ili kushughulikia tamaa yenu ya hadhi na tamaa zenu badhirifu. Matumaini, hadhi, na dhana yote ni mifano bora kabisa ya tabia ya kishetani. Sababu ambayo vitu hivi vipo katika mioyo ya watu ni kwa sababu hasa sumu ya Shetani daima inaharibu fikira za watu, na daima watu hawawezi kuondoa vishawishi hivi vya Shetani. Wanaishi katikati ya dhambi ilhali hawaiamini kuwa dhambi, na bado wao huwaza: “Tunaamini katika Mungu, hivyo lazima Atupe baraka na kupanga kila kitu kwa ajili yetu ipasavyo. Tunaamini katika Mungu, hivyo lazima tuwe wa cheo cha juu kuliko wengine, na lazima tuwe na hadhi zaidi na maisha zaidi ya baadaye kuliko mtu mwingine yeyote. Kwa kuwa tunaamini katika Mungu, lazima Atupe baraka bila kikomo. Vinginevyo, hakungeitwa kuamini katika Mungu.” Kwa miaka mingi, mawazo ambayo watu wametegemea kwa ajili ya kuendelea kuishi kwao yamekuwa yakiharibu mioyo yao hadi kiwango ambapo wamekuwa wadanganyifu, waoga, na wenye kustahili dharau. Hawakosi tu ushupavu na uamuzi, lakini pia wamekuwa walafi, wenye kiburi, na wa kudhamiria. Kabisa wanakosa uamuzi wowote upitao sana ubinafsi, na hata zaidi, hawana ujasiri hata kidogo wa kuondoa shutuma za ushawishi huu wa giza. Fikira na

maisha ya watu ni mabovu sana kiasi kwamba mitazamo yao juu ya kuamini katika Mungu bado ni miovu kwa namna isiyovumilika, na hata watu wanaponena kuhusu mitazamo yao juu ya imani katika Mungu haivumiliki kabisa kusikia. Watu wote ni waoga, wasiojimudu, wenye kustahili dharau, na dhaifu. Hawahisi maudhi kwa nguvu za giza, na hawahisi upendo kwa nuru na ukweli; badala yake, wanafanya kila wanaloweza kuvifukuza. Je, si fikira na mitazamo yenu ya sasa iko hivi tu? “Kwa kuwa ninaamini katika Mungu ninapaswa tu kumiminiwa baraka na inapaswa kuhakikishwa kwamba hadhi yangu kamwe haitelezi na kwamba inabaki kuwa juu kuliko ile ya wasioamini.” Hamjakuwa mkihodhi mtazamo wa aina hiyo ndani yenu kwa mwaka mmoja au miaka miwili tu, lakini kwa miaka mingi. Kufikiria kwenu kwa kibiashara kumekua sana. Ingawa mmewasili kwenye hatua hii leo, bado hamjaacha hadhi lakini mnapambana bila kukoma kuuliza kuihusu, na mnaichunguza kila siku, kwa hofu kubwa kwamba siku moja hadhi yenu itapotea na jina lenu litaharibiwa. Watu hawajawahi kuweka kando tamaa yao ya starehe. Hivyo, Ninapowahukumu hivi leo, mtakuwa na kiwango kipi cha ufahamu mwishowe? Mtasema kwamba ingawa hadhi yenu haiko juu, mmefurahia kuinuliwa na Mungu. Kwa sababu mmezaliwa katika tabaka la chini, hamna hadhi, lakini mnapata hadhi kwa sababu Mungu anawainua—hiki ni kitu ambacho Aliwapa. Leo mna uwezo wa kibinafsi wa kupokea mafunzo ya Mungu, kuadibu Kwake, na hukumu Yake. Huku, hata zaidi, ni kuinuliwa na Yeye. Mnaweza kupokea utakaso na kuchomwa Kwake binafsi. Huu ni upendo mkuu wa Mungu. Kupitia enzi hakujakuwa hata mtu mmoja ambaye amepokea utakaso na kuchomwa Kwake, na hakuna hata mtu mmoja ambaye ameweza kukamilishwa kwa maneno Yake. Mungu sasa Ananena nanyi ana kwa ana, Akiwatakasa, Akifichua uasi wenu wa ndani—huu kweli ni kuinuliwa na Yeye. Watu wana uwezo upi? Kama wao ni wana wa Daudi au ni uzao wa Moabu, kwa jumla, watu ni viumbe ambao hawana chochote chenye kustahili kujigamba kuhusu. Kwa kuwa nyinyi ni viumbe wa Mungu, lazima mtekeleze wajibu wa kiumbe. Hakuna mahitaji mengine kwenu. Hivi ndivyo mnavyopaswa kuomba: “Ee Mungu! Kama nina hadhi au la, sasa ninajielewa mwenyewe. Hadhi yangu ikiwa juu ni kwa sababu ya kuinuliwa na Wewe, na ikiwa iko chini ni kwa sababu ya mpango Wako. Kila kitu ki mikononi Mwako. Sina chaguzi zozote, wala malalamishi yoyote. Ulipanga kwamba ningezaliwa katika nchi hii na miongoni mwa watu hawa, na yote ninayopaswa kufanya ni kuwa mtiifu kabisa chini ya utawala Wako kwa sababu kila kitu ki ndani ya yale ambayo Umepanga. Sifikirii kuhusu hadhi; hata hivyo, mimi ni kiumbe tu. Ukiniweka kwenye shimo lisilo na mwisho, katika ziwa la moto wa jahanamu, mimi si chochote isipokuwa kiumbe. Ukinitumia, mimi ni kiumbe. Ukinikamilisha, mimi bado ni kiumbe. Usiponikamilisha, bado nitakupenda kwa sababu mimi si zaidi ya kiumbe. Mimi si chochote zaidi ya kiumbe mdogo sana aliyeumbwa na Bwana wa uumbaji, mmoja tu miongoni mwa wanadamu wote walioumbwa. Ni Wewe uliyeniumba, na sasa kwa mara nyingine tena Umeniweka katika mikono Yako ili unitumie Utakavyo. Niko tayari kuwa chombo Chako na

foili Yako kwa sababu vyote ni vile Umepanga. Hakuna anayeweza kubadili jambo hilo. Vitu vyote na matukio yote yako katika mikono Yako.” Wakati utakapofika ambapo hutafikiria tena hadhi, basi utaondokana na hilo. Hapo tu ndipo utaweza kwa kujiamini na kutafuta kwa ujasiri, na ni hapo tu ndipo moyo wako unaweza kuwa huru dhidi ya vikwazo vyovyote. Mara tu watu watakapokuwa wamenasuliwa kutoka katika mambo haya, basi hawatakuwa na shaka tena. Ni nini kinawahangaisha wengi wenu sasa hivi? Mnazuiwa daima na hadhi na mnashughulishwa daima na matarajio yenu wenyewe. Kila wakati mnayaangalia matamshi ya Mungu, mkitaka kusoma misemo inayohusu hatima ya wanadamu na kutaka kujua matarajio yenu ni yapi na hatima yenu itakuwa ipi. Mnajiuliza, “Kweli nina matarajio yoyote? Je, Mungu ameyaondoa? Mungu anasema tu kwamba mimi ni foili; basi matarajio yangu ni yapi?” Ni vigumu kwa ninyi kuweka kando matarajio na kudura yenu. Sasa nyinyi ni wafuasi, na mmepata ufahamu fulani wa hatua hii ya kazi. Hata hivyo, bado hamjaweka kando tamaa yenu ya hadhi. Wakati hadhi yenu iko juu mnatafuta vizuri, lakini wakati hadhi yenu iko chini hamtafuti tena. Baraka za hadhi daima ziko katika fikira zenu. Kwa nini watu wengi hawawezi kujiondoa katika uhasi? Je, si jibu bila shaka ni kwa sababu ya matarajio ya kuvunja moyo? Mara tu matamshi ya Mungu yanapotolewa nyinyi huharakisha kuona hadhi na utambulisho wenu kweli vikoje. Mnaipa hadhi na utambulisho kipaumbele, na kuyaweka maono katika nafasi ya pili. Katika nafasi ya tatu ni kitu mnachopaswa kuingia katika, na katika nafasi ya nne ni mapenzi ya Mungu ya sasa. Nyinyi huangalia kwanza iwapo jina la Mungu kwenu kama “foili” limebadilika au la. Mnasoma na kusoma, na mnapoona kwamba jina la “foili” limeondolewa, mnafurahi sana na kumshukuru Mungu kwa nguvu sana na kuisifu nguvu Yake kuu. Lakini mnapoona kwamba nyinyi bado ni foili, mnaadhaika na msukumo ulio mioyoni mwenu unatoweka mara moja. Kadiri unavyotafuta zaidi kwa njia hii, ndivyo utakavyovuna kidogo zaidi. Kadiri ilivyo kubwa zaidi tamaa ya mtu ya hadhi, ndivyo itabidi washughulikiwe kwa uzito zaidi na ndivyo watakavyozalimika kupitia usafishaji mkubwa. Watu kama hao hawana thamani kabisa! Lazima wshughulikiwe na wahukumiwe vya kutosha ili waachane na mambo haya kabisa. Mkifuatilia kwa njia hii mpaka mwisho, hamtavuna chochote. Wale ambao hawafuatilii uzima hawawezi kubadilishwa, na wale ambao hawana kiu ya ukweli hawawezi kupata ukweli. Hulengi kufuatilia mabadiliko ya kibinafsi na uingiaji, lakini badala yake unalenga tamaa badhirifu na vitu vinavyozuia upendo wako kwa Mungu na kukuzuia kumkaribia Yeye. Je, vitu hivyo vinaweza kukubadili? Je, vinaweza kukuleta katika ufalme? Ikiwa kusudi la kufuatilia kwako si kutafuta ukweli, basi afadhali utumie fursa hii na kurudi duniani ili kufanikiwa. Kupoteza muda wako hivi kwa kweli hakuna thamani—kwa nini ujitesa? Je, si kweli kwamba unaweza kufurahia mambo ya aina yote katika dunia hii nzuri? Pesa, wanawake warembo, hadhi, majivuno, familia, watoto, na kadhalika—je, matokeo haya ya dunia siyo mambo mazuri zaidi ambayo ungeweza kufurahia? Kuna faida gani kuzurura zurura hapa ukitafuta mahali ambapo unaweza kuwa na furaha?

Mwana wa Adamu hana pahali pa kulaza kichwa Chake, hivyo ungekuwaje na pahali pa utulivu? Angewezaje kukuumbia pahali pazuri pa utulivu? Hilo lawezekana? Kando na hukumu Yangu, leo unaweza kupokea tu mafundisho ya ukweli. Huwezi kupata faraja kutoka Kwangu na huwezi kupata kitanda cha starehe unachotamani sana usiku na mchana. Sitakupa utajiri wa duniani. Ukifuatilia kwa kweli, basi Niko tayari kukupa njia ya uzima yote, kukutaka uwe kama samaki aliyerudi majini. Usipofuatilia kwa kweli, Nitayafuta yote. Sikoyari kutoa maneno kutoka kwa kinywa Changu kwa wale ambao ni wenye tamaa ya faraja, ambao ni kama nguruwe na mbwa tu!

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

b. Nakala ya asili inasema “wake.”

Jinsi Athari za Hatua ya Pili ya Kazi ya Ushindi Zinavyotimizwa

Kazi ya watendaji huduma ilikuwa hatua ya kwanza katika kazi ya ushindi. Leo ndiyo hatua ya pili katika kazi ya ushindi. Kwa nini kukamilishwa kunatajwa pia katika kazi ya ushindi? Ni ili kujenga msingi kwa ajili ya siku za baadaye. Leo ndiyo hatua ya mwisho ya kazi ya ushindi; wakati wa kupitia dhiki kuu, ambao utaashiria mwanzo rasmi wa kuwakamilisha wanadamu, utafuata. Swala kuu sasa ni ushindi, lakini sasa pia ndio wakati wa hatua ya kwanza katika mchakato wa kukamilishwa. Kile ambacho hatua hii ya kwanza inahitaji ni kukamilisha maarifa na utii wa watu, ambavyo bila shaka vinaunda msingi wa kazi ya ushindi. Ili uweze kukamilishwa, basi lazima uwe na uwezo wa kusimama imara katikati ya dhiki ya siku za baadaye na kujitolea kabisa ili ueneze hatua inayofuata ya kazi; hii ndiyo maana ya kukamilishwa, na wakati kama huo pia ndio wakati ambapo watu wanapatwa kabisa na Mungu. Leo tunazungumza kuhusu kushindwa, ambako ni sawa na kuzungumza kuhusu kukamilishwa. Lakini kazi ambayo inafanywa leo ndiyo msingi wa kukamilishwa katika siku za baadaye; ili kukamilishwa, lazima watu wapitie dhiki, na uzoefu huu wa dhiki lazima uwe na msingi wake katika kushindwa. Ikiwa watu hawana msingi wa leo—ikiwa hawajashindwa kabisa—basi itakuwa vigumu kwao kusimama imara wakati wa hatua inayofuata ya kazi. Kushindwa pekee si kusudi la msingi. Lakini ni hatua moja tu ya ushuhuda kwa ajili ya Mungu wanapokabiliwa na Shetani. Kukamilishwa ndilo kusudi la msingi, na usipokamilishwa, basi unaweza pia kuchukuliwa kama kitu kisicho na thamani tena. Wakati tu unapokabiliwa na dhiki katika siku za baadaye ndipo kimo chako cha kweli kitakapoonekana; ambako ni kusema, ni wakati huo tu ndipo kiwango cha utakatifu wa upendo wako kwa Mungu kitakapokuwa dhahiri. Kile ambacho watu wanasema leo ni hiki: “Lazima tumtii Mungu bila kujali Anachofanya. Kwa hiyo tuko

tayari kuwa foili^[a] ambao wanaweza kudhihirisha nguvu kuu za Mungu na tabia ya Mungu. Iwe Mungu ni mwema kwetu au Yeye hutulaani, au iwe Yeye hutuhukumu, bado tunamshukuru Mungu.” Kwamba unasema hivi kunaonyesha tu kuwa una ufahamu kidogo, lakini kama ufahamu kama huo unaweza kutumika kwa kweli kunategemea kama ufahamu huu ni halisi au la. Kwamba watu wanao utambuzi na ufahamu kama huu leo ni matokeo ya kazi ya ushindi. Kama unaweza kukamilishwa au la kunaweza kuonekana tu unapokabiliwa na dhiki, na wakati huo itaonekana kama unampenda Mungu kwa kweli kwa dhati. Ikiwa upendo wako ni safi kwa kweli, basi utasema: “Sisi ni foili, sisi ni viumbe walio mikononi mwa Mungu.” Unapoieneza injili kwa watu wa mataifa, utasema, “Ninafanya huduma tu. Kwa kutumia tabia potovu zilizo ndani mwetu, Mungu amesema mambo haya yote ili Atuonyeshe tabia Yake yenye haki; Asingesema mambo kama haya, hatungeweza kumwona Mungu, wala kuelewa hekima Yake, wala kupokea wokovu mkubwa kama huu na baraka kubwa kama hizi.” Ikiwa kwa kweli una utambuzi kama huo, basi hii inatosha. Hata hivyo, hujali mambo mengi unayosema leo, nawe unaongea maneno matupu tu kwa sauti kubwa: “Sisi ni foili, watendaji huduma, tunatamani kushindwa, kuwa na ushuhuda mkubwa sana wa Mungu....” Haitoshi kusema kwa sauti tu—kusema kwa sauti hakuthibitishi kuwa una kimo; lazima uwe na ufahamu wa kweli, na lazima ufahamu wako ujaribiwe.

Kumbuka yale ambayo umepitia katika kipindi hiki cha wakati, na angalia tena maneno ambayo Nimeonyesha katika wakati huu, na uyalinganishe na yale ambayo umefanya. Ni kweli kabisa kuwa wewe ni foili kabisa! Je, kiwango cha ufahamu wako ni kipi leo? Fikira zako, mawazo yako, tabia yako, maneno na matendo yako—si kila kitu unachoonyesha katika namna unavyoishi ni foili kwa haki na utakatifu wa Mungu? Si kile kinachofunuliwa katika maneno ya leo ni tabia potovu ya mwanadamu? Fikira zako, motisha yako—yote ambayo yamefunuliwa ndani yako yanaonyesha tabia ya Mungu yenye haki na utakatifu Wake. Mungu pia Alizaliwa katika nchi ya uchafu, lakini Anabaki kutopakwa matope na uchafu. Anaishi katika ulimwengu huo huo mchafu kama wewe, lakini Anayo mantiki na utambuzi, naye huchukia uchafu. Huenda usiweze hata kugundua kitu chochote kilicho kichafu katika maneno na vitendo vyako, lakini Yeye anaweza, na Yeye hukuonyesha kitu hicho. Mambo hayo yako ya zamani—ukosefu wako wa ukuzaji, utambuzi, na akili, na njia zako za kuishi za kuelekea nyuma—sasa vimedhihirishwa na ufunuo wa leo; ni kwa Mungu kuja duniani kufanya kazi tu ndipo watu wanaona utakatifu Wake na tabia Yake yenye haki. Yeye hukuhukumu na kukuadibu, Akikusababisha upate ufahamu; wakati mwingine, asili yako ya kishetani inadhihirishwa, na Yeye hukuonyesha asili hiyo. Anajua kiini cha mwanadamu vyema sana. Yeye huishi kama unavyoishi, Yeye hula chakula kile kile kama wewe, naye Anaishi katika nyumba ileile—lakini Yeye anajua zaidi. Hakuna kitu Yeye hudharau zaidi ya falsafa za kuishi na udanganyifu na usaliti wa mwanadamu;

Yeye anadharau mambo haya na hataki kuyatilia maanani hata kidogo. Anachukia hasa maingiliano ya kimwili ya mwanadamu. Huenda Asijue baadhi ya mazoea ya maingiliano ya binadamu, lakini Anajua kabisa watu wanapofichua tabia potovu. Yeye hufanya kazi ili kuongea na kumfundisha mwanadamu kupitia mambo haya, Yeye hutumia mambo haya ili Awahukumu watu, na kuonyesha tabia Yake mwenyewe yenye haki na takatifu. Hivyo, watu wanakuwa foili kwa kazi Yake. Ni Mungu mwenye mwili tu ndiye Anayeweza kuweka wazi tabia potovu za mwanadamu na sura zote mbaya za Shetani. Kwa kufanya hivi, Yeye hakuadhibu, lakini badala yake Anakutumia tu kama foili kwa ajili ya utakatifu Wake, na huwezi kusimama imara, kwa sababu wewe ni mchafu sana. Yeye huzungumza Akitumia mambo hayo ambayo yamefunuliwa ndani ya mwanadamu, na ni wakati ambapo mambo haya yanawekwa wazi tu ndipo watu wanajua jinsi Mungu alivyo mtakatifu. Yeye hapuuzi uchafu hata kidogo ndani ya watu, hata mawazo machafu yaliyo mioyoni mwao; ikiwa maneno na matendo ya watu hayapatani na mapenzi Yake, basi Yeye hawasamehei. Katika maneno Yake, hakuna nafasi ya uchafu wa wanadamu au kitu kingine chochote—lazima yote yafunuliwe. Ni wakati huo tu ndipo utakapona kuwa kweli Yeye ni tofauti na mwanadamu. Ikiwa kuna uchafu kidogo sana ndani ya watu, basi Yeye huwachukia kabisa. Hata kuna nyakati ambapo watu hawawezi kuelewa, na wanasema, “Mungu, mbona Umekasirika sana? Mbona Wewe huzingatii udhaifu wa mwanadamu? Mbona Usiwasamehe watu kidogo? Mbona Wewe humfikirii mwanadamu hata kidogo? Ni wazi kwamba Unajua ni kwa kiwango gani ambacho watu wamepotoshwa, basi mbona bado Unawatendea hivi?” Yeye hudharau dhambi, Anachukizwa nayo, naye Anachukizwa hasa ikiwa kuna dalili yoyote ya kutotii ndani yako. Unapoonyesha tabia ya uasi, Yeye huiona naye Anachukizwa kwa kina—Anachukizwa kwa njia isiyo ya kawaida. Ni kupitia kwa mambo haya ndipo tabia Yake na kile Mungu alichu vinaonyeshwa. Ukilinganisha tabia ya Mungu na kile Mungu alichu na wewe binafsi, ulinganishi huu unaonyesha kuwa ingawa Yeye hula chakula sawa na mwanadamu, huvaa nguo sawa, hufurahia vitu anavyofurahia mwanadamu, na huishi na kukaa pamoja nao, bado Yeye ni tofauti na mwanadamu. Je, huu sio umuhimu wa foili? Ni kupitia mambo haya ya kibinadamu ndipo nguvu za Mungu zinaonyeshwa; ni giza ambalo huanzisha uwepo wa thamani wa nuru.

Bila shaka, Mungu hawafanyi muwe foili bila sababu. Badala yake, ni wakati tu kazi hii inapozaa matunda ndipo inapodhihirika kwamba uasi wa mwanadamu ni foili kwa tabia ya Mungu yenye haki, na ni kwa sababu tu ninyi ni foili ndiyo mna fursa ya kujua onyesho asili la tabia ya Mungu yenye haki. Mnahukumiwa na kuadibiwa kwa sababu ya uasi wenu, lakini ni uasi wenu pia unaowafanya muwe foili, na ni kwa sababu ya uasi wenu ndiyo mnapokea neema kubwa ambayo Mungu huwapa. Uasi wenu ni foili kwa kudura na hekima ya Mungu, na pia ni kwa sababu ya uasi wenu ndiyo mmepata wokovu na baraka nyingi kama hizo. Ingawa

mmehukumiwa nami mara kwa mara, mmepokea baraka nyingi sana ambazo hazijawahi kupokelewa na mwanadamu. Kazi hii ni ya muhimu sana kwenu. Kuwa “foili” pia ni yenye thamani sana kwenu: Mmekombolewa na kuokolewa kwa sababu ninyi ni foili, kwa hiyo foili kama huyo si wa thamani kubwa sana? Je, si mwenye umuhimu mkubwa sana? Ni kwa sababu ninyi mnaishi katika ulimwengu uleule, nchi hiyo hiyo chafu, sawa na Mungu, kwamba ninyi ni foili na mnapokea wokovu mkubwa zaidi. Mungu asingekuwa mwili, ni nani angekuwa na huruma kwenu, na ni nani angewatunza, watu duni kama ninyi? Nani angewajali? Mungu asingekuwa mwili ili Afanye kazi miongoni mwenu, mngepokea lini wokovu huu ambao wale waliokuwa kabla yenu hawakuwahi kuupata? Nisingekuwa mwili ili Niwajali, Nihukumu dhambi zenu, je, si mngelikuwa mmeanguka kuzimu kitambo? Nisingekuwa mwili na kujinyenyekeza miongoni mwenu, mngewezaje kustahili kuwa foili kwa tabia ya Mungu yenye haki? Je, ninyi si foili kwa sababu Nilichukua umbo la binadamu na kuja miongoni mwenu ili kuwawezesha kupata wokovu mkubwa zaidi? Je, hampokei wokovu huu kwa sababu Nimekuwa mwili? Mungu asingekuwa mwili ili Aishi nanyi, je, bado mngegundua kuwa mnaishi maisha ya mateso hapa duniani, ambayo ni mabaya kuliko mbwa na nguruwe? Je, hamjaadibiwa na kuhukumiwa kwa sababu ninyi ni foili kwa kazi Yangu katika mwili? Hakuna kazi inayofaa zaidi kwenu kuliko kazi ya foili, kwa kuwa ni kwa sababu ninyi ni foili ndiyo mnaokolewa katikati ya hukumu. Je, hamhisi kuwa kustahilishwa kutenda kama foili ni baraka yenu kubwa zaidi ya maisha? Ninyi hufanya kazi ya foili tu, lakini mnapokea wokovu kiasi ambacho hamjawahi kuwa nacho au hata kufikiria. Leo, jukumu lenu ni kuwa foili, na thawabu yenu ya haki ni kupokea baraka za milele katika siku za baadaye. Wokovu mnaoupata si ufahamu wa muda mfupi au ufahamu fulani wa muda kwa ajili ya wakati huu, lakini baraka kubwa zaidi: mwendelezo wa milele wa maisha. Ingawa Nimetumia “foili” kuwashinda, mnapaswa kujua kwamba wokovu na baraka hii imetolewa ili kuwapata; ni kwa ajili ya ushindi, lakini pia ni ili Niweze kuwaokoa vyema zaidi. “Foili” ni ukweli, lakini sababu ambayo ninyi ni foili ni kwa sababu ya uasi wenu, na ni kwa sababu ya jambo hili ndiyo mmepata baraka ambazo hakuna mtu amewahi kupata. Leo mnasababishwa kuona na kusikia; kesho mnapokea, na zaidi ya hayo, mtabarikiwa sana. Kwa hiyo, foili si wenye thamani kubwa sana? Athari za kazi ya leo ya ushindi zinatimizwa kupitia tabia zenu zenye uasi mkitenda kama foili. Yaani, kilele cha kuadibu na hukumu ya mara ya pili ni kutumia uchafu na uasi wenu kama foili, kukiwasababisha kuona tabia ya Mungu yenye haki. Mnapokuwa watiifu tena katika hukumu na kuadibu kwa mara ya pili, basi tabia nzima ya Mungu yenye haki inaonyeshwa wazi kwenu. Hii ni kusema kwamba wakati ambapo kukubali kwenu kazi ya ushindi kunakamilika, huu pia ndio wakati ambapo mnamaliza kutekeleza jukumu la foili. Si nia Yangu kuwapachika majina. Badala yake, Ninatumia jukumu lenu kama watendaji huduma ili kutekeleza kazi ya ushindi ya mara ya kwanza, Nikionyesha tabia ya Mungu yenye haki na isiyokosewa. Kupitia tofauti yenu, kupitia

uasi wenu mkitenda kama foili, athari za kazi ya ushindi ya mara ya pili zinatimizwa, zikiwaonyesha kikamilifu tabia ya Mungu yenye haki, ambayo haikuwa imeonyeshwa kikamilifu mara ya kwanza, na zikiwaonyesha tabia yote ya Mungu yenye haki, yote Aliyo, ambayo yanajumuisha hekima, maajabu na utakatifu wa asili wa kazi Yake. Athari ya kazi kama hiyo inatimizwa kupitia ushindi katika vipindi tofauti, na kupitia hukumu za viwango tofauti. Kadri hukumu inavyofikia kilele chake, ndivyo inavyofichua zaidi tabia za uasi za watu, na ndivyo ushindi unavyokuwa wenye kufaa zaidi. Tabia nzima ya Mungu yenye haki imewekwa wazi wakati wa kazi hii ya ushindi. Kazi ya ushindi imegawanywa katika hatua mbili, nayo ina hatua na viwango tofauti, na hivyo bila shaka, athari ambazo zinatimizwa pia ni tofauti. Hii ni kusema kwamba kiwango cha utii wa watu kinazidi kuwa kikubwa hata zaidi. Ni baada ya hii tu ndiyo watu wanaweza kuletwa kikamilifu kwenye njia sahihi ya ukamilifu; ni baada tu ya kazi yote ya ushindi kukamilishwa (wakati hukumu ya mara ya pili imetimiza athari yake ya mwisho) ndipo watu hawahukumiwi tena lakini wanaruhusiwa kuingia kwenye njia sahihi ya kupitia maisha. Kwa maana hukumu ni ishara ya ushindi, na ushindi huchukua umbo la hukumu na kuadibu.

Mungu alipata mwili katika mahali palipokuwa nyuma kimaendeleo na pachafu zaidi, na ni kwa njia hii tu ndiyo Mungu anaweza kuonyesha wazi tabia Yake yote iliyo takatifu na yenye haki. Na tabia Yake yenye haki inaonyeshwa kupitia nini? Inaonyeshwa Anapozihukumu dhambi za mwanadamu, Anapomhukumu Shetani, Anapochukia dhambi sana, na Anapowadharau maadui wanaompinga na kuasi dhidi Yake. Maneno Ninayonena leo ni kwa ajili ya kuzihukumu dhambi za mwanadamu, kuhukumu udhalimu wa mwanadamu, kulaani uasi wa mwanadamu. Upotovu na udanganyifu wa mwanadamu, maneno na vitendo vya mwanadamu—yote ambayo hayapatani na mapenzi ya Mungu lazima yatapitia hukumu, na uasi wa mwanadamu kushutumiwa kama dhambi. Maneno Yake yanahusu kanuni za hukumu; Yeye hutumia hukumu ya udhalimu wa mwanadamu, laana ya uasi wa mwanadamu, na mfichuo wa asili mbaya za mwanadamu ili kudhihirisha tabia Yake mwenyewe yenye haki. Utakatifu ni kielelezo cha tabia Yake yenye haki, na kwa kweli utakatifu wa Mungu ni tabia Yake yenye haki. Tabia zenu potovu ni muktadha wa maneno ya leo—Ninazitumia kunena na kuhukumu, na kutekeleza kazi ya ushindi. Hii pekee ndiyo kazi halisi, na hii pekee inadhihirisha kabisa utakatifu wa Mungu. Ikiwa hakuna dalili ya tabia potovu ndani yako, basi Mungu hatakuhukumu, wala hatakuonyesha tabia Yake yenye haki. Kwa kuwa unayo tabia potovu, Mungu hatakusamehe, na ni kwa njia hii ndiyo utakatifu Wake unaonyeshwa. Mungu angaliona kuwa uchafu na uasi wa mwanadamu vilikuwa vikubwa sana lakini Asinene au kukuhukumu, wala kukuadibu kwa ajili ya udhalimu wako, basi hii ingethibitisha kwamba Yeye si Mungu, kwa maana Asingeichukia dhambi; Angelikuwa mchafu sawasawa na mwanadamu. Leo, ni kwa sababu ya uchafu wako ndiyo Ninakuhukumu, na ni kwa sababu ya upotovu na uasi wako ndiyo Ninakuadibu. Mimi sijivunii

nguvu Zangu kwenu au kuwadhulumu kwa makusudi; Ninafanya mambo haya kwa sababu ninyi, ambao mmezaliwa katika nchi hii ya uchafu, mmenajisiwa vikali kwa uchafu. Mmepoteza uadilifu na ubinadamu wenu kabisa na mmekuwa kama nguruwe waliozaliwa katika pembe chafu zaidi za ulimwengu, na kwa hiyo ni kwa sababu ya jambo hili ndiyo mnahukumiwa na ndiyo Ninawaachia huru hasira Yangu. Ni kwa sababu hasa ya hukumu hii ndiyo mmeweza kuona kuwa Mungu ndiye Mungu mwenye haki, na kwamba Mungu ndiye Mungu mtakatifu; ni kwa sababu hasa ya utakatifu Wake na haki Yake ndiyo Anawahukumu na kuachia huru hasira Yake juu yenu. Kwa sababu Anaweza kufichua tabia Yake yenye haki Aonapo uasi wa mwanadamu, na kwa sababu Anaweza kufichua utakatifu Wake anapona uchafu wa mwanadamu, hii inatosha kuonyesha kuwa Yeye ndiye Mungu Mwenyewe ambaye ni mtakatifu na wa asili, na bado Anaishi katika nchi ya uchafu. Mungu angelikuwa mtu na kufuata mfano wa mwanadamu na kugaaga na wanadamu katika matope machafu, basi kusingelikuwa na chochote kitakatifu kumhusu, na Asingelikuwa na tabia yenye haki, na kwa hiyo Asingelikuwa na haki ya kuhukumu uovu wa mwanadamu, wala Asingelikuwa na haki ya kutekeleza hukumu ya mwanadamu. Mtu angelimhukumu mtu mwingine, haingekuwa kana kwamba anajipiga kofi usoni? Watu ambao wote ni wachafu kwa kiwango sawa wanastahili vipi kuwahukumu wale ambao ni sawa na wao? Ni Mungu mtakatifu Mwenyewe pekee ndiye Anayeweza kuwahukumu wanadamu wote wachafu. Mwanadamu angewezaje kuhukumu dhambi za mwanadamu? Mwanadamu angewezaje kuona dhambi za mwanadamu, na mwanadamu angewezaje kuwa na sifa za kulaani dhambi hizi? Mungu Asingelikuwa na sifa ya kuzihukumu dhambi za mwanadamu, basi Angewezaje kuwa Mungu mwenye haki Mwenyewe? Tabia potovu za watu zinapofichuliwa, Mungu hunena ili Awahukumu watu, na ni hapo tu ndipo watu wanapona kuwa Yeye ni mtakatifu. Anapomhukumu na kumwadibu mwanadamu kwa ajili ya dhambi zake, wakati huo wote Akizifichua dhambi za mwanadamu, hakuna mtu au kitu kinachoweza kuepuka hukumu hii; mambo yote ambayo ni machafu yanahukumiwa na Yeye, na ni kwa sababu hiyo tu ndiyo tabia Yake inaweza kusemwa kuwa yenye haki. Kama ingekuwa vinginevyo, ingewezaje kusemwa kwamba ninyi ni foili kwa jina na kwa kweli?

Kuna tofauti kubwa kati ya kazi iliyofanywa Israeli na kazi ya leo. Yehova aliyaongoza maisha ya Waisraeli, na hakukuwa na kuadibu na hukumu nyingi, kwa sababu wakati huo, watu walielewa kidogo sana kuhusu ulimwengu na walikuwa na tabia chache zilizokuwa potovu. Hapo zamani, Waisraeli walimtii Yehova kabisa. Alipowaambia wajenge madhabahu, walijenga madhabahu haraka; Alipowaambia wavae mavazi rasmi ya makuhani, walitii. Katika siku hizo, Yehova alikuwa kama mchungaji akilichunga kundi la kondoo, na kondoo wakifuata mwongozo wa mchungaji na kula nyasi katika malisho; Yehova aliyaongoza maisha yao, Akiwaongoza katika jinsi walivyokula, kuvalia, kuishi, na kusafiri. Huo haukuwa wakati wa kuweka wazi tabia

ya Mungu, kwa kuwa wanadamu wa wakati huo walikuwa waliozaliwa karibuni; kulikuwa na wachache waliokuwa waasi na wapinzani, hakukuwa na uchafu mwingi kati ya wanadamu, na kwa hivyo watu hawangeweza kutenda kama foili kwa tabia ya Mungu. Ni kupitia watu ambao wanatoka katika nchi ya uchafu ndipo utakatifu wa Mungu unaonyeshwa; leo, Yeye hutumia uchafu ulioonyeshwa katika watu hawa wa nchi ya uchafu, naye Anahukumu, na kwa kufanya hivyo, kile Alichokinafichuliwa katika hukumu Yake. Kwa nini Anahukumu? Anaweza kunena maneno ya hukumu kwa sababu Anadharau dhambi; Je, Angewezaje kukasirika sana hivyo ikiwa hakuchukia uasi wa wanadamu? Kusingekuwa na karaha ndani Yake, kusingekuwa na machukio, Asingejali uasi wa watu, basi hiyo ingethibitisha Yeye kuwa mchafu kama mwanadamu. Kwamba Yeye anaweza kumhukumu na kumwadibu mwanadamu ni kwa sababu Yeye huchukia uchafu, na Anachokichukia hakimo ndani Yake. Kama pia kungekuwa na upinzani na uasi ndani Yake, Asingewadharau wale ambao ni wapinzani na waasi. Kazi ya siku za mwisho ingekuwa ikifanywa Israeli, hakungekuwa na maana yoyote kwayo. Mbona kazi ya siku za mwisho inafanywa nchini China, mahali paovu na palipo nyuma kabisa kimaendeleo kuliko sehemu zote? Ni ili kuonyesha utakatifu na haki Yake. Kwa kifupi, kadri mahali palivyo paovu, ndivyo utakatifu wa Mungu unavyoweza kuonyeshwa wazi zaidi. Kwa kweli, yote haya ni kwa ajili ya kazi ya Mungu. Ni leo tu ndipo mnatambua kuwa Mungu ameshuka kutoka mbinguni ili Asimame kati yenu, Ameonyeshwa kupitia uchafu na uasi wenu, na ni wakati huu tu ndipo mnamjua Mungu. Je, hii siyo sifa kubwa zaidi? Kwa kweli, ninyi ni kikundi cha watu nchini China waliochaguliwa. Na kwa sababu mlichaguliwa na mmefurahia neema ya Mungu, na kwa sababu hamfai kufurahia neema kubwa kama hiyo, hii inathibitisha kwamba haya yote ni kuwapa sifa kubwa kabisa. Mungu amewatokea, na kuwaonyesha tabia Yake nzima iliyo takatifu, na Amewapa yote hayo, na kuwasababisha mfurahie baraka zote ambazo mnaweza kufurahia. Hamjaionja tu tabia ya Mungu yenye haki, lakini, zaidi ya hayo, mmeuonja wokovu wa Mungu, ukombozi wa Mungu na upendo wa Mungu usio na kikomo. Ninyi, wachafu zaidi ya wote, mmefurahia neema kubwa kama hii—je, hamjabarikiwa? Je, huku si Mungu kuwainua? Ninyi ni wa chini zaidi ya wote, kwa asili hamstahili kufurahia baraka kubwa kama hiyo, lakini Mungu anang'ang'ania kukuinua. Je, huoni aibu? Ikiwa huwezi kutekeleza wajibu wako, basi mwishowe utaaibika, nawe utajiadhibu. Leo, hufundishwi nidhamu, wala huadhibiwi; mwili wako uko salama salimini—lakini mwishowe, maneno haya yatakuaibisha. Hadi leo, bado Sijamwadibu mtu yeyote waziwazi; maneno Yangu yanaweza kuwa makali, lakini Ninawatendeaje watu? Ninawafariji, na kuwashawishi, na kuwakumbusha. Ninafanya hivi ili kuwaokoa tu. Je, kwa kweli hamwelewi mapenzi Yangu? Mnapaswa kuelewa Ninachosema, na kutiwa moyo nacho. Ni sasa tu ndipo kunao watu wengi wanaoelewa. Je, hii si baraka ya kuwa foili? Je, kuwa foili si jambo la kubarikiwa zaidi? Mwishowe, mnapoenda kueneza injili, mtasema hivi: “Sisi ni foili wa kawaida.” Watawauliza, “Inamaanisha nini kwamba ninyi ni foili

wa kawaida?” Nanyi mtasema: “Sisi ni foili kwa kazi ya Mungu, na kwa nguvu Zake kuu. Tabia nzima ya Mungu yenye haki imefunuliwa kupitia uasi wetu; sisi ni vyombo vya kutumikia kwa kazi ya Mungu ya siku za mwisho, sisi ni viambatisho vya kazi Yake, na pia vifaa vya kazi hiyo.” Wanaposikia hivyo, watavutiwa sana. Baadaye, utasema: “Sisi ni vielelezo na mifano ya Mungu kukamilisha kazi ya ulimwengu wote, na ya ushindi Wake wa wanadamu wote. Iwe sisi ni watakatifu au wachafu, kwa jumla, bado tumebarikiwa zaidi kuliko ninyi, kwa maana tumemwona Mungu, na kupitia fursa ya Yeye kutushinda, nguvu kuu za Mungu zimeonyeshwa; ni kwa sababu tu sisi ni wachafu na waovu ndiyo tabia Yake yenye haki imetokea. Je, hivyo mnaweza kuishuhudia kazi ya Mungu ya siku za mwisho? Hamstahili! Hii ni Mungu kutuinua tu! Ingawa tunaweza kukosa kuwa wenye kiburi, tunaweza kumsifu Mungu kwa kujivunia, kwa kuwa hakuna mtu anayeweza kurithi ahadi kubwa kama hiyo, na hakuna mtu anayeweza kufurahia baraka kubwa kama hiyo. Tunashukuru sana kwamba sisi, ambao ni wachafu sana, tunaweza kufanya kazi kama foili wakati wa usimamizi wa Mungu.” Na wanapouliza, “Vielelezo na mifano ni nini?” unasema, “Sisi ni wanadamu waasi zaidi na wachafu zaidi; tumepotoshwa kwa kina kabisa na Shetani, nasi ni viumbe tulio nyuma kimaendeleo na duni zaidi kimwili. Sisi ni mifano bora ya wale ambao wametumiwa na Shetani. Leo, tumechaguliwa na Mungu kama wa kwanza kati ya wanadamu walioshindwa, na tumeona tabia ya Mungu yenye haki na kurithi ahadi Yake; tunatumiwa kuwashinda watu zaidi, kwa hiyo sisi ndio vielelezo na mifano ya wale wanaoshindwa kati ya wanadamu.” Hakuna ushuhuda bora zaidi kuliko maneno haya, na huu ndio uzoefu wako bora kabisa.

Tanbihi:

a. Foili: Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Ukweli wa Ndani wa Kazi ya Ushindi (2)

Mlikuwa mnatafuta kutawala kama wafalme, na leo bado hamjaacha kabisa suala hili; bado mnatamani kutawala kama wafalme, kushikilia mbingu na kuhimili dunia. Sasa, fikiria kuhusu hilo: Je, unazo sifa kama hizo? Je, huoni unakuwa mtu mpumbavu? Je, mnachokitafuta na kujitolea umakini wenu kwacho ni cha uhalisi? Hamna hata hali ya kawaida ya ubinadamu—hilo si la kusikitisha? Hivyo, leo Nazungumzia tu juu ya kushindwa, kuwa na ushuhuda, kuendeleza ubora wa tabia yako, na kuingia katika njia ya kufanywa kuwa mkamilifu, na kutozungumzia kitu chochote kile. Watu wengine wanaonekana kuchoshwa na ukweli usiotiwa doa, na wanapoona mazungumzo haya yote ya ubinadamu wa kawaida na kuendeleza ubora wa tabia ya watu, wanakaidi. Wale ambao hawapendi ukweli sio rahisi kuwafanya wakamilifu. Ili mradi mnaingia leo, na kutenda kulingana na mapenzi ya Mungu, hatua kwa hatua, je, utaweza kuondolewa? Baada ya Mungu kufanya kazi nyingi sana katika eneo bara la Uchina—kazi ya

kiwango kikubwa hivyo—na baada ya Yeye kuzungumza maneno mengi sana, je, Angesalimu amri Akiwa katikati? Je, angewapeleka watu kuzimu? Kitu ambacho ni cha msingi leo ni kwamba lazima mjue hulka ya mwanadamu, na lazima mjue ni nini mnapaswa kuingia kwacho; unapaswa kuzungumza juu ya kuingia katika maisha, na mabadiliko katika tabia, jinsi ya kushindwa kwa kweli, na jinsi ya kumtii Mungu kabisa, kuwa na ushuhuda wa Mungu wa mwisho, na kutimiza utii hata kifo. Unapaswa kulenga mambo haya, na kile ambacho si chenye uhalisi au muhimu kinapaswa kuwekwa pembeni na kisizingatiwe. Leo, unapaswa kuelewa namna ya kushindwa, na jinsi watu wanavyofanya baada ya kushindwa. Unaweza kusema umeshashindwa, lakini unaweza kutii hata kufa? Unapaswa uwe na uwezo wa kufuata hadi mwisho kabisa bila kujali kama kuna matumaini yoyote, na hupaswi kupoteza imani kwa Mungu bila kujali mazingira. Mwishowe, unapaswa kutimiza hali mbili za ushuhuda: ushuhuda wa Ayubu—utii hata kifo—na ushuhuda wa Petro—upendo mkuu wa Mungu. Kwa upande mmoja, unapaswa kuwa kama Ayubu: Hakuwa na mali hata kidogo, na alisumbuliwa na maumivu ya mwili, lakini hakulikana jina la Yehova. Huu ulikuwa ushuhuda wa Ayubu. Petro aliweza kumpenda Mungu hadi kifo. Alipokufa—alipoangikwa msalabani—bado alimpenda Mungu; hakufikiria juu ya matarajio yake mwenyewe au kufuatilia mambo yaliyo makuu au fikra za anasa, na alitafuta tu kumpenda Mungu, na kutii mipango yote ya Mungu. Hicho ndicho kiwango unachopaswa kutimiza kabla hujahesabiwa kuwa na ushuhuda, kabla hujawa mtu ambaye amefanywa mkamilifu baada ya kushindwa. Leo, ikiwa watu wangukuwa wanajua kabisa hulka na hadhi yao, je, bado wangetafuta matarajio yao na matumaini yao? Unachopaswa kujua ni hiki: Bila kujali kama Mungu atanifanya mkamilifu, ni lazima nimfuate Mungu; kila kitu anachofanya sasa ni chema na kinafanywa kwa ajili yangu, na ili tabia yetu iweze kubadilika na tuweze kuepukana na ushawishi wa Shetani, kuturuhusu kuzaliwa katika nchi ya uchafu na hata hivyo kuepukana na uchafu, kuondoa uchafu na ushawishi wa Shetani, kutuwezesha kuacha nyuma ushawishi wa Shetani. Bila shaka, hiki ndicho unachotakiwa kuwa nacho, lakini kwa Mungu ni ushindi tu, ili watu wawe na azimio la kutii, na waweze kutii mipango yote ya Mungu. Kwa njia hii, mambo yatakamilishwa. Leo, watu wengi tayari wamekwishashindwa, lakini ndani yao bado kuna mengi ambayo ni ya uasi na ukaidi. Kimo cha kweli cha watu bado ni kidogo sana, na wao huwa na nguvu kamili ikiwa kuna matumaini na matarajio, kama hayapo, wanakuwa na mitazamo hasi, na hata wanafikiria kuhusu kumwacha Mungu. Na watu hawana shauku kuu ya kutafuta kuishi kulingana na maisha ya ubinadamu wa kawaida. Hilo halitafaulu. Hivyo, bado lazima Nizungumze juu ya ushindi. Kwa kweli, ukamilifu hutokea wakati mmoja na ushindi: Unaposhindwa, matokeo ya kwanza ya kufanywa mkamilifu pia yanatimizwa. Panapokuwa na tofauti kati ya kushindwa na kufanywa mkamilifu, ni kulingana na kiwango cha mabadiliko kwa watu. Kushindwa ni hatua ya kwanza ya kufanywa mkamilifu, na haimaanishi kwamba wamefanywa wakamilifu kabisa, wala kuthibitisha kwamba wamepatwa na Mungu kabisa.

Baada ya watu kushindwa, kunakuwa na mabadiliko fulani katika tabia yao, lakini mabadiliko hayo ni pungufu sana yakilinganishwa na mabadiliko ya watu ambao wamepatwa kabisa na Mungu. Leo, kile kinachofanywa ni kazi ya mwanzo ya kuwafanya watu kuwa wakamilifu—kuwashinda—na kama huwezi kutimiza kushindwa, basi hutaweza kuwa na uwezo wa kufanywa mkamilifu na kupatwa kabisa na Mungu. Utapata tu maneno machache ya kuadibu na hukumu, lakini hayatakuwa na uwezo wa kuubadilisha kabisa moyo wako. Hivyo utakuwa mmoja wa wale ambao wameondolewa; haitakuwa tofauti na kutazama tu karamu ya gharama mezani lakini huli. Je, hilo si la huzuni? Na hivyo, ni lazima utafute mabadiliko: Kama ni kushindwa au kufanywa mkamilifu, yote yanahusiana na kama kuna mabadiliko ndani yako, na kama wewe ni mtii au la, na hili linaamua kama unaweza kupatwa na Mungu au la. Jua kwamba “kushindwa” na “kufanywa mkamilifu” yamejikita katika kiwango cha mabadiliko na utii, vilevile katika jinsi upendo wako kwa Mungu ulivyo. Kinachotakiwa leo ni kwamba uweze kufanywa mkamilifu kabisa, lakini mwanzoni ni lazima ushindwe—ni lazima uwe na ufahamu wa kutosha juu ya kuadibu na hukumu ya Mungu, lazima uwe na imani ya kufuata, na kuwa mtu ambaye anatafuta mabadiliko na matokeo kuweko. Wakati huo tu ndipo utakuwa mtu ambaye anatafuta kufanywa mkamilifu. Unapaswa kuelewa kwamba wakati wa kufanywa kuwa mkamilifu, mtashindwa, na wakati wa kushindwa mtafanywa kuwa wakamilifu. Leo, unaweza kutafuta kufanywa kuwa mkamilifu au kutafuta mabadiliko katika ubinadamu wako wa nje na maendeleo katika ubora wa tabia yako, lakini muhimu kabisa ni kwamba unaweza kuelewa kwamba kila kitu ambacho Mungu anafanya leo kina maana na ni cha manufaa: Kinakuwezesha wewe ambaye unazaliwa katika nchi ya uchafu kuepuka uchafu na kuuondoa wote, kinakuwezesha kushinda ushawishi wa Shetani na kuacha nyuma ushawishi wa giza wa Shetani—na kwa kulenga vitu hivi, unakuwa umelindwa katika nchi hii ya uchafu. Mwishowe, utaambiwa utoe ushuhuda gani? Unazaliwa katika nchi ya uchafu lakini unaweza kuwa mtakatifu, usichafuliwe na najisi tena, unamilikiwa na Shetani, lakini unaachana na ushawishi wa Shetani, na humilikiwi au kunyanyaswa na Shetani, na unaishi mikononi mwa Mwenyezi. Huu ndio ushuhuda, na thibitisho la ushindi katika vita na Shetani. Unaweza kumwacha Shetani, hufichui tabia za kishetani tena katika kile unachoishi kwa kudhihirisha, lakini badala yake unaishi kwa kudhihirisha kile ambacho Mungu alitaka mwanadamu afikie Alipomuumba mwanadamu: ubinadamu wa kawaida, urazini wa kawaida, umaizi wa kawaida, azimio la kawaida la kumpenda Mungu, na utii kwa Mungu. Huo ndio ushuhuda ambao kiumbe wa Mungu huwa nao. Unasema, “Tunazaliwa katika nchi ya uchafu, lakini kwa sababu ya ulinzi wa Mungu, kwa sababu ya uongozi Wake, na kwa sababu Ametushinda, tumejiondoa katika ushawishi wa Shetani. Kwamba tunaweza kutii leo pia ni matokeo ya kushindwa na Mungu, na sio kwa sababu sisi ni wema, au kwa sababu tunampenda Mungu kwa asili. Ni kwa sababu Mungu alituchagua, na kutujaalia, ndio tumeshindwa leo, tunaweza kuwa na ushuhuda Kwake, na tunaweza kumhudumia, kwa hiyo, pia, ni kwa sababu

Alituchagua, na kutulinda, ndio tumechaguliwa na kutolewa katika miliki ya Shetani, na tunaweza kuachana na uchafu na kutakaswa katika nchi ya joka kuu jekundu.” Aidha, kile unachoishi kwa kudhihirisha nje kitaonyesha kwamba una ubinadamu wa kawaida, kuna maana katika kile unachosema, na unaishi kwa kudhihirisha mfano wa mtu wa kawaida. Watu wengine wanapokuona, hupaswi kuwasababisha waseme, “Je, hii siyo sura ya joka kuu jekundu?” Matendo ya dada hayaonekani kuwa ni ya dada, matendo ya kaka hayaonekani kuwa ni ya kaka, na huna staha yoyote ya watakatifu.” Kisha watu wanaweza kusema, “si ajabu Mungu alisema ni uzao wa Moabu, Alikuwa sahihi kabisa!” Ikiwa watu wanawatazama na kusema, “Ingawa Mungu alisema wewe ni uzao wa Moabu, kile unachokiishi kwa kudhihirisha kimethibitisha kwamba umeachana na ushawishi wa Shetani; ingawa mambo hayo bado yapo ndani yako, unaweza kuachana nayo,” basi hili linaonyesha kwamba umeshindwa kabisa, wewe ambaye umeshindwa na kuokolewa utasema, “Ni kweli kwamba sisi ni uzao wa Moabu, lakini tumeokolewa na Mungu, na ingawa uzao wa Moabu ulikataliwa na kulaaniwa, na kupelekwa uhamishoni na Waisraeli miongoni mwa Mataifa, leo Mungu ametuokoa. Ni kweli kwamba sisi ni wapotovu kuliko watu wote—hili lilitamkwa na Mungu, huu ni ukweli, na haupingwi na mtu yeyote. Lakini leo tumeukwepa ushawishi huo. Tunawachukia sana mababu zetu, tupo radhi kuwageuzia migongo mababu zetu, kuwatelekeza kabisa na kutii mipango yote ya Mungu, kutenda kulingana na mapenzi ya Mungu, na kutimiza matakwa Yake kwetu, na kufikia ridhaa ya mapenzi ya Mungu. Moabu alimsaliti Mungu, hakutenda kulingana na mapenzi ya Mungu, na alichukiwa na Mungu. Lakini tunapaswa kujali moyo wa Mungu, na leo, kwa kuwa tunaelewa mapenzi ya Mungu, hatuwezi kumsaliti Mungu, na tunapaswa kuwakana mababu zetu wa kale!” Hapo awali Nilizungumza juu ya kumkana joka kuu jekundu—na leo, huko ni kukana hasa mababu wa kale. Huu ni ushuhuda mmoja wa ushindi wa watu, na bila kujali ni jinsi gani unaingia leo, ushuhuda wako katika eneo hili haupaswi kukosekana.

Ubora wa tabia ya watu ni duni sana, wanapungukiwa sana na ubinadamu wa kawaida, kupokea kwao ni kwa polepole sana, kwa uvivu, uharibifu wa Shetani umewaacha wakiwa wapumbavu, na ingawa hawawezi kubadilika kabisa kwa kipindi cha mwaka mmoja au miwili, ni lazima wawe na azimio la kushiriki. Inaweza kusemwa kuwa huu pia ni ushuhuda mbele ya Shetani. Ushuhuda wa leo ni matokeo yaliyotimizwa na kazi ya sasa ya ushindi, vilevile kama sampuli na mfano wa kuigwa na wafuasi wa baadaye. Hapo baadaye, utaenea katika mataifa yote; kile kinachofanyika Uchina kitaenea katika mataifa yote. Uzao wa Moabu ni watu duni sana kuliko watu wote duniani. Watu wengine huuliza, je, wafuasi wa Hamu sio duni kuliko wote? Kizazi cha joka kuu jekundu na uzao wa Hamu ni wenye umuhimu tofauti wakilishi, na uzao wa Hamu ni suala jingine. Bila kujali ni jinsi gani wamelaaniwa, bado ni uzao wa Nuhu; asili za Moabu, wakati ule ule, hazikuwa safi: Moabu alitoka katika uzinzi, na hii ndiyo tofauti.

Ingawa wote walilaaniwa, hali zao hazikuwa sawa, na kwa hiyo uzao wa Moabu ni watu duni kabisa kuliko wote—hakuna ukweli unaoweza kushawishi kuliko kushindwa kwa watu duni kuliko watu wote. Kazi ya siku za mwisho inavunja kanuni zote, bila kujali kama umelaaniwa au kuadhibiwa, maadamu tu uisaidie kazi Yangu, na una manufaa kwa kazi ya ushindi ya leo, na bila kujali kama wewe ni uzao wa Moabu au kizazi cha joka kuu jekundu, maadamu tu unatekeleza wajibu wa kiumbe wa Mungu katika hatua hii ya kazi, na kufanya kadri unavyoweza, basi matokeo yanayotarajiwa yatatimizwa. Wewe ni kizazi cha joka kuu jekundu, na ni uzao wa Moabu; kwa ujumla, wale wote walio wa mwili na damu ni viumbe wa Mungu, na waliumbwa na Muumba. Wewe ni kiumbe wa Mungu, hupaswi kuwa na chaguo lolote, na huu ndio wajibu wako. Bila shaka, leo kazi ya Muumba imeelekezwa kwa ulimwengu mzima. Bila kujali wewe ni uzao wa nani, zaidi ya yote, nyinyi ni mojawapo wa viumbe wa Mungu, ninyi—uzao wa Moabu—ni sehemu ya viumbe wa Mungu, ni vile tu nyinyi mna thamani ya chini. Kwa kuwa, leo, kazi ya Mungu inatekelezwa miongoni mwa viumbe wote, na imelenga ulimwengu mzima, Muumba yuko huru kuchagua watu, masuala, au vitu vyovyote ili viweze kufanya kazi Yake. Hajali wewe ni uzao wa nani; maadamu tu wewe ni mmoja wa viumbe wake, na maadamu una manufaa katika kazi Yake—kazi ya ushindi na ushuhuda—Ataifanya kazi Yake ndani yako bila haya yoyote. Hili linaharibu kabisa dhana za watu za kitamaduni, ambayo ni kwamba Mungu hatawahi kamwe kufanya kazi miongoni mwa Mataifa, hususan wale ambao wamelaaniwa na ambao ni duni; kwa maana wale ambao wamelaaniwa, uzao wao wa baadaye nao utaendelea kulaaniwa milele, hawatakuwa na nafasi ya wokovu; Mungu hatawahi kamwe kushuka na kufanya kazi katika nchi ya Mataifa, na Hatakanyaga mguu Wake katika nchi yenye uchafu, maana Yeye ni mtakatifu. Dhana hizi zote zimevunjwa na kazi ya Mungu katika siku za mwisho. Jua kwamba Mungu ni Mungu wa viumbe vyote, ni mtawala wa mbingu na nchi na vitu vyote, na si Mungu wa watu wa Israeli pekee. Hivyo, kazi hii katika nchi ya Uchina ni ya umuhimu mkubwa, na unadhani haitaenea miongoni mwa mataifa yote? Ushuhuda mkubwa wa siku za usoni hautakomea Uchina tu; ikiwa Mungu angewashinda nyinyi tu, je, mapepo wangeshawishika? Hawaelewi maana ya kushindwa, au nguvu kubwa ya Mungu, na ni pale tu ambapo wateuliwa wa Mungu katika nchi yote watakapoona matokeo ya mwisho ya kazi hii ndipo viumbe wote watakuwa wameshindwa. Hakuna ambao wapo nyuma sana au waovu sana kuliko uzao wa Moabu. Iwapo tu watu hawa wataweza kushindwa—wale ambao ni waovu sana, ambao hawakumtambua Mungu au kuamini kwamba kuna Mungu wameshindwa, na kumtambua Mungu katika vinywa vyao, wakimtukuza, na wanaweza kumpenda—ndipo huu utakuwa ushuhuda wa ushindi. Ingawa wewe si Petro, mnaishi kwa kudhihirisha mfano wa Petro, mnaweza kuwa na ushuhuda wa Petro, na ushuhuda wa Ayubu, na huu ni ushuhuda mkubwa sana. Hatimaye utasema: “Sisi sio Waisraeli, bali ni uzao wa Moabu uliotelekezwa, sisi sio Petro, ambaye hatuwezi kuwa na ubora wa tabia yake, wala sisi sio Ayubu, na hata hatuwezi

kujilinganisha na azimio la Paulo la kuteseka kwa ajili ya Mungu na kujitoa kikamilifu kwa Mungu, na sisi tupo nyuma sana, na hivyo, hatustahili kufurahia baraka za Mungu. Mungu bado Ametuinua leo; kwa hiyo tunapaswa kumridhisha Mungu, na ingawa tuna ubora wa tabia au sifa haba, tupo radhi kumridhisha Mungu—tuna azimio hili. Sisi ni uzao wa Moabu, na tulilaaniwa. Hili lilitangazwa na Mungu, na wala hatuwezi kuibadilisha, lakini kuishi kwetu kwa kudhihirisha na maarifa yetu yanaweza kubadilika, na tumeazimia kumridhisha Mungu.” Utakapokuwa na azimio hili, itathibitisha kwamba umeshuhudia kuwa umeshindwa.

Ukweli wa Ndani wa Kazi ya Ushindi (3)

Matokeo ya kutimizwa kutoka kwa kazi ya kushinda kimsingi ni kwa ajili ya mwili wa mwanadamu kuacha kuasi, yaani, ili fikira za mwanadamu zipate ufahamu mpya wa Mungu, moyo wake umtii Mungu kabisa, na aamue kuwa wa Mungu. Watu hawahesabiwi kuwa walioshindwa wakati ambapo ambapo mwenendo ama mwili wao unapobadilika; wakati ambapo fikira, ufahamu, na utambuzi wa mwanadamu unabadilika, ambayo ni kusema, wakati ambapo mwelekeo wako wote wa akili unabadilika—huo utakuwa wakati ambapo umeshindwa na Mungu. Ukiamua kutii na kupata fikira mpya, pale ambapo huingizi mawazo na nia zako katika maneno na kazi ya Mungu, na wakati ubongo wako unaweza kufikiri kwa njia ya kawaida, yaani, unapoweza kujitolea kwa Mungu kwa moyo wako wote—huyu ni mtu aliyeshindwa kabisa. Katika ulimwengu wa dini, watu wengi huteseka pakubwa maishani mwao mwote, kwa kuihini miili yao au kuubeba msalaba wao, au hata kuteseka na kustahimili hadi pumzi zao za mwisho! Wengine huwa wanafunga hadi siku ya kifo chao. Katika maisha yao yote wanajinyima chakula kizuri na mavazi mazuri, wakisisitiza mateso tu. Wanaweza kuihini miili yao na kuinyima miili yao. Uwezo wao wa kustahimili mateso unastahili sifa. Ila fikira zao, mawazo yao, mielekeo yao ya kiakili, na kwa hakika asili yao ya kale, havijashughulikiwa hata kidogo. Hawana ufahamu wowote wa kweli kujihusu. Picha ya Mungu akilini mwao ni ile ya kijadi na ya kidhahania, Mungu asiye yakini. Uamuzi wao wa kuteseka kwa ajili ya Mungu unaletwa na azma na asili yao chanya. Hata ikiwa wanamwamini Mungu, hawamfahamu Mungu wala kuyafahamu mapenzi Yake. Wanamfanyia Mungu kazi na kumtesekea Mungu kama vipofu. Hawawekei utambuzi thamani yoyote na hawajishughulishi na jinsi ambayo huduma yao inatimiza mapenzi ya Mungu kwa kweli. Aidha hawajui jinsi ya kutimiza ufahamu kuhusu Mungu. Mungu wanayemhudumia si Mungu katika sura Yake ya asili, ila ni Mungu waliyejifikiria, Mungu waliyemsikia, au Mungu wa kihadithi wanayemsoma katika maandiko. Kisha wanatumia mawazo yao dhahiri na mioyo yao ya kiungu kumtesekea Mungu na kuifanya kazi ambayo Mungu anapaswa kufanya. Huduma yao haiko sahihi, kiasi kwamba hakuna yeyote kati yao anayeweza kuhudumu kulingana na mapenzi ya Mungu. Haijalishi wako radhi kiasi gani kuteseka, mitazamo yao asilia ya huduma na picha ya Mungu akilini mwao havibadiliki kwani hawajapitia hukumu ya Mungu

na kuadibu na usafishaji Wake na ukamilifu, na kwa sababu hakuna yeyote aliyewaongoza na ukweli. Japo wanasadiki kwa Yesu Mwokozi, hamna kati yao aliyewahi kumwona Mwokozi. Wamemsikia tu kwa hadithi na uvumi. Hivyo huduma yao ni sawa na kuhudumu mara mojamocha macho yao yakiwa yamefungwa kama kipofu anayemhudumia baba yake. Ni nini kinaweza kupatikana kutokana na huduma kama hiyo? Na ni nani anaweza kuikubali? Huduma yao haibadiliki kamwe toka mwanzo hadi mwisho. Wanapokea mafunzo ya kibinadamu na kukita huduma yao katika uasili wao na kile wanachokipenda wao. Hili laweza kuzalisha faida gani? Hata Petro, aliyemwona Yesu, hakujua jinsi ya kumhudumia Mungu kwa njia inayotimiza mapenzi ya Mungu. Ni katika uzee wake ndipo alipopata ufahamu. Hili linaonyesha nini kuhusu wanadamu vipofu ambao hawajapitia ushughulikiaji na hawana upogoaji na ambao hawajawahi kupata yeyote wa kuwaongoza? Je, si huduma ya wengi miongoni mwenu leo ni kama ile ya vipofu? Wale wote ambao hawajapokea hukumu, hawajapokea upogoaji na ushughulikiaji, na hawana mabadiliko—je, wao si waliokosa kushindwa kabisa? Wana manufaa gani watu kama hao? Ikiwa fikira zako, ufahamu wako wa maisha, na ufahamu wako wa Mungu hauonyeshi mabadiliko mapya na hautoi faida hata kidogo, hutatimiza chochote kizuri katika huduma yako. Bila maono na bila ufahamu mpya wa kazi ya Mungu, huwezi kuwa mtu aliyeshindwa. Njia yako ya kumfuata Mungu itakuwa kama ile ya wale wanaoteseka na kufunga—itakuwa ya thamani ndogo! Hii ni kwa sababu kuna ushuhuda kidogo katika yale wayafanyayo ndipo Nasema huduma yao ni bure! Wanashinda maisha yao wakiteseka na kukaa gerezeni; ni wastahimilivu, wenye upendo daima na wao daima hubeba msalaba, wao hukejeliwa na kukataliwa na dunia, wao hupitia kila aina ya ugumu, na ingawa wao ni watiifu hadi mwisho kabisa, bado hawajashindwa, na hawawezi kutoa ushuhuda kuhusu kushindwa.. Wameteseka si haba, ila kwa ndani hawamfahamu Mungu kabisa. Hakuna fikira zao za zamani, mawazo ya zamani, vitendo vyao, uelewa wa wanadamu, na mawazo ya wanadamu yaliyoshughulikiwa. Kamwe hakuna uelewa mpya ndani yao. Hakuna hata chembe ya ufahamu wao wa Mungu ambao ni wa kweli au ni sahihi. Wamekosa kuyaelewa mapenzi ya Mungu. Je, huku kwaweza kuwa kumhudumia Mungu? Japo ulimfahamu Mungu zamani, tuseme umeudumisha ufahamu huo hadi leo na kuendelea kukita ufahamu wako kuhusu Mungu kwenye fikira na mawazo yako bila kujali Mungu anafanya nini. Yaani, ikiwa huna ufahamu mpya na wa kweli kuhusu Mungu na ukose kutambua sura na tabia ya kweli ya Mungu. Ikiwa ufahamu wako wa Mungu bado unaongozwa na fikira za uhasama na ushirikina na bado una mawazo na fikira za mwanadamu. Ikiwa hii ndiyo hali, basi hujashindwa. Lengo langu la kukwambia maneno haya yote sasa ni kukupa fursa ya kufahamu na kutumia utambuzi huu kukuongoza katika ufahamu sahihi na mpya. Aidha yanalengwa kukuondolea mawazo ya zamani na utambuzi wa zamani ulio nao ili uweze kuwa na ufahamu mpya. Ikiwa unakula na kunywa matamshi Yangu kweli, basi ufahamu wako utabadilika kwa kiwango kikubwa. Bora tu udumishe moyo mtiifu kwa kula na kunywa

matamshi ya Mungu, mtazamo wako utabadilika. Bora tu unaweza kukubali kuadibu kwa kila mara, fikira zako za zamani zitabadilika taratibu. Bora tu fikira zako za zamani zimebadilishwa kabisa na kuwa mpya, vitendo vyako vitabadilika ipasavyo. Kwa njia hii, huduma yako itaendelea kuwa yenye malengo zaidi, na itaweza kutimiza mapenzi ya Mungu. Kama unaweza kubadilisha maisha yako, ufahamu wako wa maisha ya binadamu, na mawazo yako mengi kuhusu Mungu, basi uasili wako utadidimia taratibu. Hili, na hakuna jingine ila hili, ndilo tokeo baada ya Mungu kumshinda mwanadamu; haya ndiyo mabadiliko yatakayoonekana ndani ya mwanadamu. Ikiwa katika kumwamini Mungu, yote ujuayo ni kuutiisha na kuuhini mwili wako na kustahimili na kuteseka, na hujui wazi ikiwa unachokifanya ni sawa au la, bila kujali unamfanyia nani kazi, basi vitendo kama hivi vitaletaje mabadiliko?

Mnapaswa kufahamu kuwa Ninachokitarajia kutoka kwenu si kwamba miili yenu iwekwe katika kifungo au bongo zenu zitawaliwe na kuzuiwa kufikiria mawazo dhahania. Hili si lengo la kazi wala kazi inayopaswa kufanywa hivi sasa. Hivi sasa mnahitaji kuwa na ufahamu kutoka kwa mtazamo chanya ili muweze kubadilika wenyewe. Kile mnachohitaji kufanya zaidi ni kujiandaa wenyewe na maneno ya Mungu, kumaanisha kujiandaa kwa ukamilifu na ukweli na maono yaliyo mbele yenu sasa, na kisha mwende mbele na kuyatia katika vitendo. Hili ni jukumu lenu. Siwaambii mtafute na kupata hata mwangaza mkuu zaidi. Kwa sasa ninyi hamna kabisa kimo cha hilo. Kinachohitajika kutoka kwenu ni kufanya yote muwezayo ili kula na kunywa maneno ya Mungu. Mnatakiwa kufahamu kazi ya Mungu na mjue asili yenu, uwezo wenu, na yale maisha yenu ya zamani. Hususan mnapaswa kujua kuhusu vile vitendo vyenu vyenye makosa vya zamani na mienendo yenu ya kibinadamu. Ili Kubadilika, mnapaswa kuanza kwa kubadilisha fikira zenu. Kwanza, badilisha fikira zenu za zamani kwa fikira mpya, na mruhusu fikira zenu mpya ziongoze maneno na matendo yenu na maisha yenu. Hili ndilo ombi kwa kila mtu sasa hivi. Msitende kama kipofu au kufuata kama kipofu. Ni sharti muwe na msingi na lengo. Msijidanganye. Mnapaswa mjue kabisa imani yenu kwa Mungu ni kwa ajili ya nini, ina faida gani, na kitu gani mnachopaswa kuingia kwacho sasa hivi. Ni muhimu kwamba uyafahamu haya yote.

Kile mnachopaswa kuingia ndani sasa hivi ni kuyainua maisha yenu na kukweza uhodari wenu. Kuongezea, mnahitaji kubadilisha hiyo mitazamo ya zamani kutoka kwa siku zenu za zamani, mbadilishe kufikiri kwenu, na mbadilishe fikira zenu. Maisha yenu yote yanahitaji kufanywa upya. Ufahamu wako wa matendo ya Mungu unapobadilika, unapokuwa na ufahamu mpya wa ukweli wa kila anachokisema Mungu, na ufahamu wako wa ndani unapoinuliwa, maisha yako yanabadilika na kuwa bora. Kila kitu kinachofanywa na kusemwa na mwanadamu sasa ni cha utendaji. Haya si mafundisho ya dini, ila kile ambacho watu wanahitaji kwa ajili ya maisha yao na kile wanachopaswa kumiliki. Hili ndilo badiliko linalotokea kwa mwanadamu

wakati wa kazi ya kushinda, badiliko ambalo mwanadamu anapaswa kupitia, na ndiyo matokeo baada ya mwanadamu kushindwa. Ukishabadilisha fikira zako, uchukue mwelekeo mpya wa kimawazo, ubadilishe mawazo yako na nia zako na mantiki yako ya zamani, uache mambo yaliyokita mizizi ndani yako, na kupata ufahamu mpya wa imani kwa Mungu, basi, ushuhuda unaotoa utainuliwa na uwepo wako mzima, kwa kweli utakuwa umebadilika. Yote haya ndiyo ya kiutendaji zaidi, halisi zaidi, na vitu vya kimsingi kabisa—vituvilivyokuwa vigumu kwa mwanadamu kuelewa hapo zamani, na hawakuweza kushughulika navyo. Ndiyo kazi ya kweli ya Roho. Ni vipi hasa ulivyoelewa Biblia zamani? Ulinganishi wa haraka leo utakwambia. Zamani ulikweza Musa, Petro, Paulo, au kauli na mitazamo hiyo yote ya Biblia. Sasa, kama ungeambiwa uikweze Biblia, ungefanya hivyo? Ungeona kwamba Biblia ina rekodi nyingi sana zilizoandikwa na mwanadamu na kwamba Biblia ni maelezo tu ya hatua mbili za kazi ya Mungu. Ni kitabu cha historia. Je, hili halina maana kwamba ufahamu wako kuihusu umebadilika? Kama ungeangalia sasa ukoo wa Yesu uliotolewa katika Injili ya Mathayo, ungesema, “Ukoo wa Yesu? Upuuzi! Huu ni ukoo wa Yusufu, si wa Yesu. Hakuna uhusiano kati ya Yesu na Yusufu.” Unapoiangalia Biblia sasa, ufahamu wako kuihusu ni tofauti, kumaanisha mtazamo wako umebadilika, na unaleta ufahamu wa kiwango cha juu zaidi kwayo kuliko wasomi wa dini wa zamani. Mtu fulani anaposema kwamba kuna kitu katika ukoo huu, ungejibu, “Ni nini kiko hapo? Endelea na ufafanue. Yesu na Yusufu hawana uhusiano. Je, hulijui hilo? Je, Yesu anaweza kuwa na ukoo? Yesu anawezaje kuwa na mababu? Anawezaje kuwa uzao wa mwanadamu? Mwili wake ulizaliwa na Maria; Roho Wake ni Roho wa Mungu, si roho ya mwanadamu. Yesu ni Mwana mpendwa wa Mungu, kwa hiyo anaweza kuwa na ukoo? Wakati alipokuwa duniani Hakuwa mshirika wa wanadamu, kwa hiyo Anawezaje kuwa na ukoo?” Unapochambua ukoo na kufafanua ukweli kwa dhahiri, ukishiriki kile ambacho umeelewa, mtu huyo ataachwa ameduwaa. Watu wengine watarejelea Biblia na kukuuliza, “Yesu alikuwa na ukoo. Je, Mungu wako wa leo ana ukoo?” Wewe basi utawaambia ufahamu wako wenye uhalisi zaidi. Kwa njia hii, ufahamu wako utakuwa umepata matokeo. Kwa kweli, Yesu hana uhusiano na Yusufu kabisa na hata zaidi hana uhusiano na Abrahamu. Ni kwamba tu Yesu alizaliwa Israeli. Lakini Mungu si Mwisraeli au uzao wa Waisraeli. Kwa vile tu Yesu alizaliwa Israeli, haimaanishi Mungu ni Mungu wa Waisraeli pekee. Ilikuwa tu kwa kusudi la kazi Yake ndio Alichukua hii hatua ya kupata mwili Mwenyewe. Mungu ni Mungu wa viumbe vyote ulimwenguni. Ni vile tu kwanza Alifanya hatua moja ya kazi katika Israeli na kisha, baadaye, Akaanza kufanya kazi katika nchi za Mataifa. Lakini watu walimdhania Yesu kuwa Mungu wa Waisraeli na zaidi ya hayo walimweka miongoni mwa Waisraeli na miongoni mwa vizazi vya Daudi. Biblia inasema kwamba mwishoni mwa siku, jina la Yehova litakuwa kuu miongoni mwa nchi za Mataifa, kumaanisha Mungu atakuwa akifanya kazi ndani ya nchi za Mataifa katika siku za mwisho. Kwamba alipata mwili Uyahudini wakati huo wa zamani hakuashirii kwamba Mungu

anawapenda Wayahudi pekee. Hilo lilitendeka tu kwa sababu kazi ililihitaji. Haiwezi kusemwa kwamba Mungu alitakiwa kupata mwili ndani ya Israeli (kwa sababu Waisraeli walikuwa wateule Wake). Je, wateule wa Mungu hawapatikani katika nchi za Mataifa, pia? Ni baada ya Yesu kumaliza kufanya kazi Uyahudi ndiyo kazi ikapanuka hadi kwa nchi za Mataifa. (Waisraeli waliziita nchi zote nje ya Israeli “nchi za Mataifa.”) Kwa kweli, hizo nchi za Mataifa zilijazwa wateule wa Mungu vilevile; ni kwamba tu hakuna kazi iliyokuwa ikifanywa huko wakati huo. Watu hutilia mkazo kama huo kwa Israeli kwa sababu hatua mbili za kwanza za kazi zilifanyika Israeli ilhali hakuna kazi iliyokuwa ikifanyika katika nchi za Mataifa. Kazi katika nchi za Mataifa inanza tu leo, na ndiyo maana watu wanaona ugumu kuikubali. Kama unaweza kuelewa kwa dhahiri haya yote, uyakubali sawasawa na kuyatazama mambo haya yote kwa sahihi, utakuwa na ufahamu sahihi wa Mungu wa leo na wa zamani, na utakuwa wa juu zaidi kuliko ufahamu wa Mungu uliomilikiwa na watakatifu kotekote katika historia. Kama wewe hupitia kazi ya leo na kusikia matamko ya Mungu binafsi leo, lakini huna ufahamu kabisa wa ukamili wa Mungu; ukimbizaji wako ukibaki kama ulivyokuwa daima na usibadilishwe na kitu chochote kipya; na hasa ukipitia kazi hii yote ya kushinda, lakini hatimaye hakuna mabadiliko yoyote yanaweza kuonekana ndani yako, basi imani yako si kama ile ya wale ambao hutafuta tu mkate kushibisha njaa yao? Kwa hiyo, kazi ya kushinda haitakuwa imetimiza matokeo yo yote ndani yako. Basi wewe hutakuwa mtu wa kutolewa?

Katika hitimisho la kazi yote ya kushinda, ni muhimu kwamba nyinyi nyote mfahamu kwamba Mungu si Mungu wa Israeli tu, ila ni Mungu wa kila kiumbe. Aliumba wanadamu wote wala si Waisraeli tu. Ukisema kuwa Mungu ni Mungu wa Israeli tu au kwamba haiwezekani Mungu kupata mwili katika taifa lolote lililo nje ya Israeli, basi bado hujafikia ufahamu wowote katika harakati ya kazi ya kushinda na hutambui kamwe kwamba Mungu ni Mungu wako. Kile unachokitambua ni kuwa Mungu alitoka Israeli Akaenda Uchina na Analazimishwa kuwa Mungu wako. Iwapo huu ndio mtazamo wako wa vitu, basi kazi Yangu haijazaa matunda ndani yako na hujaelewa chochote Nilichokisema. Hatimaye, ikiwa utaandika ukoo Wangu, sawa na Mathayo, Nitafutie babu afaaye na Nitafutie mizizi sahihi—ili kwamba Mungu ana koo mbili kwa sababu ya kupata Kwake mwili mara mbili—je, huo hautakuwa mzaha mkubwa zaidi duniani? Wewe “mtu mwenye nia njema” uliyenipatia ukoo, je, huwezi kuwa mtu uliyemgawa Mungu? Je, uko tayari kuubeba mzigo huu wa dhambi? Baada ya hii kazi yote ya kushinda, ikiwa huamini kwamba Mungu ni Mungu wa viumbe wote, ikiwa bado unadhani kwamba Mungu ni Mungu wa Waisraeli tu, je, wewe si mtu anayemkana Mungu waziwazi? Kusudi la kukushinda leo ni kukufanya utambue kuwa Mungu ni Mungu wako, na Mungu wa wengine, na muhimu zaidi ni Mungu wa wote wanaompenda, na Mungu wa viumbe wote. Ni Mungu wa Israeli na Mungu wa Misri. Ni Mungu wa Waingereza na Mungu wa Wamarekani. Si Mungu wa

Adamu na Hawa tu, bali pia Mungu wa kizazi cha Adamu na Hawa. Ni Mungu wa kila Kitu mbinguni na duniani. Familia ya Waisraeli na familia zote za Mataifa zimo mikononi mwa Mungu. Hakufanya kazi katika nchi ya Israeli pekee kwa miaka elfu kadhaa na kuzaliwa Uyahudi, ila leo Anashuka Uchina, nchi hii ambapo joka kuu jekundu limejikunja. Ikiwa kuzaliwa Uyahudi kunamfanya Mfalme wa Wayahudi, basi si kushuka kwake miongoni mwenu leo kunamfanya Mungu wenu? Aliwaongoza Waisraeli na alizaliwa Yudea na vilevile amezaliwa katika nchi ya Mataifa. Je, kazi Yake yote haifanywi kwa ajili ya wanadamu wote Aliowaumba? Je, Anawapenda Waisraeli mara mia moja na kuwachukia Mataifa mara elfu moja? Je, hayo siyo mawazo yenu? Ni ninyi ambao hamtambui Mungu; si kwamba Mungu Hakuwa Mungu wenu. Ni ninyi mnaomkataa Mungu; si kwamba Mungu hapendi kuwa Mungu wenu. Ni nani kati ya walioumbwa hayuko mikononi mwa mwenye Uweza? Kwa kuwashinda leo, je, lengo si kuwafanya mtambue kuwa Mungu ni Mungu wenu? Iwapo bado mnashikilia kuwa Mungu ni Mungu wa Waisraeli tu, na kuendelea kushikilia kuwa nyumba ya Daudi huko Israeli ni asili ya uzao wa Mungu na kuwa hakuna taifa tofauti na Israeli limewezeshwa “kumzaa” Mungu, na hata zaidi kuwa hakuna familia ya Mataifa yenye uwezo wa kupokea kazi ya Yehova—ikiwa bado unafikiria hivi, je, haikufanyi kuwa mshikiliaji wa ukaidi? Usikazie macho Israeli kila wakati. Mungu Yuko hapa miongoni mwenu leo. Vilevile msitazamie mbingu tu. Acheni kutamani Mungu wenu Aliye mbinguni! Mungu ametua miongoni mwenu, basi Anawezaje kuwa mbinguni? Hujaamini katika Mungu kwa muda mrefu, ilhali una mawazo mengi kuhusu Mungu, kiasi kwamba unathubutu kutofikiri hata kwa sekunde moja kuwa Mungu wa Waisraeli Anaweza kuwatunukia na uwepo wake. Wala hamthubutu kufikiri jinsi mnavyoweza kumwona Mungu Akijitokeza binafsi, ikitiliwa maanani jinsi mliyoy wachafu. Aidha hamjawahi kufikiri jinsi Mungu anavyoweza kushuka miongoni mwa Mataifa. Anapaswa kushuka juu ya Mlima Sinai au Mlima wa Mizeituni na kuonekana kwa Waisraeli. Je, si watu wa Mataifa (yaani watu wa nje ya Israeli) ndio walengwa wa chuki Yake? Anawezaje kufanya kazi miongoni mwao? Haya yote ni mawazo yaliyokita mizizi ndani yenu ambayo mmeyakuza kwa miaka mingi. Kusudi la kuwashinda leo ni kuyaharibu haya mawazo yenu. Kwa njia hiyo mmeweza kumwona Mungu akijionyesha Mwenyewe miongoni mwenu—si katika Mlima Sinai au Mlima wa Mizeituni, bali miongoni mwa watu ambao Hajawahi kuwaongoza hapo awali. Baada ya Mungu kufanyia hatua mbili za kazi Yake Israeli, Waisraeli na watu wa Mataifa walishikilia wazo hili: Japo ni kweli Mungu aliumba viumbe wote, yuko radhi kuwa Mungu wa Waisraeli tu, si Mungu wa Mataifa. Waisraeli wanaamini yafuatayo: Mungu anaweza tu kuwa Mungu wetu, sio Mungu wenu Mataifa, na kwa sababu humchi Yehova, Yehova—Mungu wetu—Anawachukia. Zaidi, Wayahudi hao huamini hili: Bwana Yesu alichukua sura yetu Wayahudi na ni Mungu aliye na alama ya Wayahudi. Mungu anafanyia kazi miongoni mwetu. Sura ya Mungu na sura zetu zinafanana; sura zetu na sura ya Mungu zinakaribiana. Bwana Yesu ni Mfalme wetu Wayahudi;

watu wa Mataifa hawajawezeshwa kupokea wokovu mkubwa kiasi hicho. Bwana Yesu ni sadaka ya dhambi kwetu Wayahudi. Ni kwa misingi ya hatua hizi mbili za kazi ndipo Waisraeli na Wayahudi walijijengea haya mawazo mengi. Wanamdai Mungu kuwa wao tu, bila kukubali kwamba Mungu vilevile ni Mungu wa Mataifa. Kwa njia hii, Mungu alikuwa pengo katika mioyo ya watu wa Mataifa. Hii ni kwa sababu kila mtu aliamini kuwa Mungu hataki kuwa Mungu wa watu wa Mataifa na kuwa Anawapenda tu Waisraeli—Wateule wake—na Anawapenda Wayahudi hasa wafuasi waliomfuata. Je, wajua kuwa kazi aliyoifanya Yehova na Yesu ilikuwa ni kwa ajili ya uzima wa wanadamu wote? Je, sasa unatambua kuwa Mungu ni wa wale wote waliozaliwa nje ya Israeli? Je, Mungu Hayumo miongoni mwenu leo? Hii haiwezi kuwa ndoto, ama vipi? Je, hamkubali uhalisi huu? Mnathubutu kutoamini au kulifikiria. Licha ya jinsi mnavyolitazama, je, Mungu hayumo miongoni mwenu? Je, bado mnaogopa kuyaamini maneno haya? Kuanzia leo, je, wote walioshindwa, na wale wote wanaotaka kuwa wafuasi wa Mungu, si wateule wa Mungu? Je, nyote mlio wafuasi leo, si wateule nje ya Israeli? Je, nafasi yenu si sawa na ya Waisraeli? Je, hili silo mnalopaswa kutambua? Je, hili si lengo la kazi ya kukushinda? Kwa kuwa mwaweza kumwona Mungu, basi Atakuwa Mungu wenu milele, tangu mwanzo hadi siku za baadaye. Hatawaacha, mradi tu nyinyi nyote mko radhi Kumfuata na kuwa viumbe Wake waaminifu na watiifu.

Haijalishi azimio lao la sasa la kumpenda Mungu ni imara vipi, mwanadamu kwa jumla amekuwa mtiifu na kufuata mpaka siku hii. Si mpaka mwisho, wakati ambapo hatua ya kazi hii itahitimishwa, ndiyo mwanadamu atatubu kabisa. Huo ndio wakati ambapo watu watashindwa kweli. Hivi sasa wako tu katika mchakato wa kushindwa. Wakati ambapo kazi itahitimishwa, watashindwa kabisa, lakini sio hivyo sasa hivi! Hata kama kila mtu ataridhika, hilo halina maana kwamba wameshindwa kabisa. Hii ni kwa kuwa kwa sasa watu wameona maneno pekee na sio matukio yenye ukweli, na wao bado hujiona wasio na hakika haijalishi vile wanavyoamini kwa kina. Ndiyo maana ni kwa hilo tukio lenye ukweli la mwisho, maneno kuwa hakika, ndiyo watu watashindwa kabisa. Hivi sasa watu hawa wanashindwa kwa sababu wanasikia kuhusu mafumbo mengi ambayo hawakuwahi kusikia kabla. Lakini ndani ya kila mmoja wao, wao bado wanatafuta na kungoja matukio fulani yenye ukweli yanayowaruhusu kuona kila neno la Mungu likitimilizwa. Ni wakati huo tu ndiyo wataridhishwa kabisa. Wakati ambao tu, mwishowe, wote wameona uhalisi huu wenye ukweli uliotimilizwa, na uhalisi huu umewasababisha kuwa na uhakika, ndiyo wataonyesha kusadiki sana ndani ya mioyo yao, kunena kwao, na macho yao, na ndiyo wataridhishwa kabisa kwa dhati. Hii ni asili ya mwanadamu. Mnahitaji kuona maneno yote yakitokea kuwa kweli, mnahitaji kuona baadhi ya matukio yenye ukweli yakitendeka na kuona msiba ukiwafika baadhi ya watu, na kisha mtaridhishwa kabisa ndani yenu. Kama Wayahudi, mnaendelea kutilia maanani sana kuona ishara na miujiza. Lakini mnaendelea kukosa

kuona kwamba kuna ishara na miujiza na kwamba uhalisi unatendeka ambao unatakiwa kuyafungua macho yenu sana. Kama ni mtu fulani anayeshuka kutoka angani, au mhimili wa mawingu ukinena kwenu, au Mimi kutekeleza upungaji pepo kwa mmoja wenu, au sauti Yangu kunguruma kama radi kati yenu, ninyi daima mmetaka na daima mtataka kuona aina hii ya tukio. Mtu anaweza kusema kwamba katika kumwamini Mungu, matakwa yenu makuu zaidi ni kumwona Mungu akija na kuwaonyesha binafsi ishara. Kisha mtaridhika. Ili kuwashinda ninyi watu, lazima Nitekeleze kazi iliyo sawa na uumbaji wa dunia na kisha kuongeza ishara. Halafu, mioyo yenu itashindwa kabisa.

Ukweli wa Ndani wa Kazi ya Ushindi (4)

Kukamilishwa kuna maana gani? kushindwa kuna maana gani? Ni vigezo vipi mtu anapaswa kuwa navyo ili apate kushindwa? Na ni vigezo vipi mtu anapaswa kuwa navyo ili afanywe mkamilifu? Kushinda na kukamilisha yote yanakusudiwa kumkamilisha mwanadamu ili kwamba aweze kurejeshwa katika asili yake, na awe huru na tabia zake potovu za shetani na ushawishi wa Shetani. Huu ushindi huja mapema katika mchakato wa kumfinyanga mwanadamu, ikiwa na maana kwamba ni hatua ya kwanza ya kazi. Kukamilisha ni hatua ya pili, au hitimisho la kazi. Kila mwanadamu ni lazima apitie hali ya kushindwa; la sivyo hataweza kumfahamu Mungu na hawezi kujua kuwa kuna Mungu, yaani, hawezi kumtambua Mungu. Na iwapo mtu hamtambui Mungu, hataweza kufanywa mkamilifu na Mungu kwa sababu hatakuwa na vigezo vya kufanywa mkamilifu. Ikiwa humtambui Mungu, utawezaje kumfahamu? Utawezaje kumtafuta? Aidha, hutaweza kumshuhudia, wala kumtosheleza. Kwa hivyo, kila anayetaka kukamilishwa, hatua ya kwanza lazima iwe kupitia kazi ya kushinda. Hili ndilo sharti la kwanza. Ila, iwe ni kushinda au ukamilifu, kila moja ni lengo la mwanadamu afanyaye kazi na kubadilishwa na kazi hiyo, na kila moja ni kipengele katika kazi ya kusimamia mwanadamu. Hizi hatua mbili ndizo zinahitajika kumgeuza yeyote kuwa mtu mkamilifu; hakuna moja kati ya hizo inaweza kurukwa. Ni kweli kuwa “kushindwa” hakuonekani kuwa ni jambo zuri, ila ni kweli kuwa mchakato wa kumshinda mtu ni mchakato wa kumbadilisha. Baada ya wewe kushindwa, tabia yako potovu huenda ikawa haijafutwa kabisa, lakini utakuwa umeijua. Kupitia kazi ya kushinda, utapata kujua uduni wa ubinadamu wako, na vilevile kufahamu utovu wako wa nidhamu. Japo hutaweza kuyaacha haya au kuyabadilisha ndani ya muda mfupi wa kazi ya kushinda, utayajua baadaye. Haya yanaujenga msingi wa ukamilifu wako. Kwa hivyo kushinda na kukamilisha yote yanafanywa kumbadilisha mwanadamu, kumtoa mwanadamu tabia zake mbovu za Kishetani ili ajitolee kikamilifu kwa Mungu. Ni kwamba tu kushindwa ni hatua ya kwanza katika kubadilisha tabia ya mwanadamu na pia hatua ya kwanza ya mwanadamu kujitoa kikamilifu kwa Mungu, hatua iliyo chini ya ukamilifu. Tabia za maisha ya mtu aliyeshindwa hubadilika kiasi kidogo kuliko ya mtu ambaye amepata ukamilifu. Kushindwa na kufanywa

mkamilifu ni tofauti kabisa kwa kuwa ni hatua tofauti za kazi na kwa kuwa huhitaji vigezo tofauti kutoka kwa wanadamu, huku ushindi ukiwa na vigezo vya chini na ukamilifu ukiwa na vigezo vya juu. Walio wakamilifu ni wenye haki, watu watakatifu na safi; wao ni udhihirisho wa kazi ya kusimamia wanadamu, au matokeo ya mwisho. Japo si wanadamu wasio na doa, ni watu wanaotaka kuishi maisha ya thamani. Lakini walioshindwa hukiri tu kwa vinywa vyao kuwa Mungu Yupo; wanakiri kuwa Mungu amepata mwili, kwamba neno linaonekana katika mwili, na kwamba Mungu amekuja duniani kufanya kazi ya hukumu na kuadibu watu. Aidha wanakiri kuwa hukumu na kuadibu kwa Mungu na mapigo Yake na usafishaji Wake ni faida kwa mwanadamu. Yaani, wameanza kuwa na sifa za ubinadamu, na wana ufahamu mdogo kuhusu maisha ila si bayana. Kwa maneno mengine, wameanza tu kuwa na ubinadamu. Haya ni matokeo ya kushindwa. Watu waingiapo katika njia ya ukamilifu, tabia zao za zamani zaweza kubadilishwa. Aidha, maisha yao huendelea kukua na taratibu hujitosa zaidi katika ukweli. Wanaweza kuchukia dunia na kuwachukia wale wote ambao hawafuati ukweli. Hususan hujichukia wao wenyewe, na hata zaidi ya hayo, wanajitambua vyema. Wana hiari kuishi kulingana na ukweli na hulenga kufuata ukweli. Hawako radhi kuishi katika mawazo ya bongo zao, na huchukia kujitukuza, kujisifu, na kujiinua kwa mwanadamu. Wananena kwa adabu ya hali ya juu, wanafanya mambo kwa utambuzi na hekima, ni waaminifu na watiifu kwa Mungu. Wakipitia kuadibu na hukumu, wao hawakuwi wanyonge au wasioonyesha hisia tu, bali hutoa shukrani kwa ajili ya kuadibu na hukumu zitokazo kwa Mungu. Wanaamini hawawezi kuishi bila kuadibu na hukumu ya Mungu; wanaweza kupata ulinzi Wake kupitia haya. Hawafuati imani ya amani na furaha na ya kutafuta mkate wa kuwashibisha. Wala hawafuati raha za muda za kimwili. Hili ndilo wakamilifu huwa nalo. Baada ya watu kushindwa, wao hukubali kwamba kuna Mungu. Lakini matendo yo yote ambayo huja na kukubali kuweko kwa Mungu, matendo haya ni machache ndani yao. Neno kuonekana katika mwili lina maana gani kwa kweli? Kupata mwili kuna maana gani? Ni nini ambacho Mungu mwenye mwili amefanya? Ni nini lengo na umuhimu wa kazi Yake? Baada ya kupitia kazi Yake nyingi sana, kupitia matendo Yake katika mwili, umepata nini? Ni baada tu ya kufahamu mambo haya yote ndiyo utakuwa mtu aliyeshindwa. Kama wewe utasema tu kwamba unakubali kuwa kuna Mungu, lakini huwachi kile unachopaswa kuwacha na kukosa kuacha raha za mwili ambazo unapaswa kuacha, lakini badala yake uendeleo kutamani maliwazo ya mwili kama ulivyofanya daima, na ikiwa huwezi kuachilia ubaguzi wowote dhidi ya ndugu, na kuhusu utendaji mwingi rahisi huwezi kulipa stahili yako kutimiza matendo hayo, basi hilo linathibitisha wewe bado hujashindwa. Kwa hiyo, hata kama unaelewa mengi, yote itakuwa bure. Walioshindwa ni watu ambao wametimiza mabadiliko fulani ya mwanzo na kuingia kwa mwanzo. Kupitia hukumu na kuadibu kwa Mungu huwasababisha kuwa na maarifa ya mwanzo ya Mungu na ufahamu wa mwanzo wa ukweli. Hata kama kuhusu ukweli mwingi wa kina, na wa chembechembe zaidi huwezi kuingia kabisa katika

uhalisi wake, unaweza kutia katika vitendo ukweli mwingi wa mwanzo katika maisha yako halisi, kama vile unaohusu raha zako za mwili au hali yako binafsi. Yote haya, bila shaka, ni kile kinachotimizwa ndani ya wale wanaopitia kushinda. Mabadiliko fulani katika tabia yanaweza pia kuonekana ndani ya walioshindwa. Kwa mfano, mavazi na unadhifu wao na maisha yao—haya yanaweza kubadilika. Mtazamo wao kuhusu kumwamini Mungu hubadilika, wao hupata uwazi kuhusu chombo cha ukimbizaji wao, na matamania yao huongezeka. Wakati wa kushindwa, tabia yao ya maisha inaweza pia kubadilika kwa kukubaliana. Sio kwamba wao hawabadiliki kabisa. Ni vile tu mabadiliko yao ni ya juujuu, ya mwanzo, na madogo zaidi kuliko mabadiliko katika tabia na chombo cha ukimbizaji ambayo yangeonekana baada ya mtu kukamilishwa. Kama wakati wa kushindwa, tabia ya mtu haibadiliki kabisa na hapati hata ukweli kidogo, basi mtu wa aina hii huwa tu kipande cha takataka na ni bure kabisa! Watu ambao hawajashindwa hawawezi kukamilishwa! Na kama mtu hutafuta tu kushindwa, hawezi kufanywa kuwa kamili kwa ukamilifu, hata kama tabia yake ilionyesha mabadiliko fulani ya kukubaliana wakati wa kazi ya kushinda. Yeye pia atapoteza ukweli wa mwanzo aliopata. Kuna tofauti kubwa mno kati ya kiasi cha mabadiliko ya tabia ndani ya walioshindwa na waliokamilishwa. Lakini kushindwa ni hatua ya kwanza katika mabadiliko; ni msingi. Kukosa mabadiliko haya ya mwanzo ni thibitisho kwamba mtu kwa kweli hamjui Mungu kabisa kwa sababu ufahamu huu hutoka kwa hukumu, na hukumu hii ni kipengee kikuu katika kazi ya kushinda. Kwa hiyo, kila mtu aliyekamilishwa amepitia kushindwa. Ama sivyo, hangeweza labda kukamilishwa.

Unasema kwamba unatambua Mungu mwenye mwili na unatambua kuwa Neno laonekana katika mwili, na bado unafanya mambo fulani bila Yeye kujua, mambo ambayo yanaenda kinyume na kile Anachotaka, na moyoni mwako humwogopi. Je, huku ni kumtambua Mungu? Unatambua Anachokisema ila unakataa kuyaweka katika vitendo hata yale mambo unayoweza kufanya na huzifuati njia zake. Je, huku ni kumtambua? Unamtambua ila mawazo yako ni kujikinga dhidi Yake, kutomcha kamwe. Ikiwa umeona na kuitambua kazi Yake na unafahamu kuwa Yeye ni Mungu, na bado unaendelea kuwa vuvuwaa na bado hujabadilika hata kidogo, basi wewe ni aina ya mtu ambaye bado hajashindwa kabisa. Wale ambao wameshindwa lazima wafanye yote wawezayo, na ingawa hawawezi kuingia katika ukweli wa juu zaidi, na ukweli huu huenda ukawashinda, watu kama hawa wako tayari moyoni mwao kufikia hili. Ni kwa sababu kuna mipaka kwa kile wanachoweza kukubali, kuna mipaka na vikomo kwa kile wanachoweza kutenda. Hata hivyo angalau, ni lazima wafanye yote wawezayo, na ikiwa unaweza kufikia hilo, haya ni matokeo ambayo yametimizwa kwa sababu ya kazi ya ushindi. Huenda ukasema, “Kwa sababu Anaweza kunena maneno mengi ambayo mwanadamu hawezi, ikiwa si Mungu, ni nani?” Kuwa na mawazo kama haya hakumaanishi unamtambua Mungu. Ikiwa unamtambua Mungu, unapaswa kuonyesha hilo kupitia kwa matendo yako halisi. Ukiongoza kanisa lakini usiweze

kutenda haki, na kutamani pesa na kufuja pesa za kanisa kisiri kwa faida yako—je, huku ni kutambua kuwa kuna Mungu? Mungu ni mwenye Uweza na wa kumcha. Unawezaje kukosa kuogopa kama kweli unatambua kuwa kuna Mungu? Unawezaje kuwa ulifanya kitu cha kuchukiza namna hiyo? Je, huko kunaweza kuitwa kuamini? Je, kweli wamtambua Mungu? Ikiwa unaweza kufanya jambo la kudharauliwa kama hilo, je, huko kweli ni kumtambua Yeye? Je, unamwamini Mungu? Unayemwamini ni Mungu asiye yakini; ndiyo maana huogopi! Wale wote wanaomtambua Mungu kweli na kumfahamu wanamcha na wanaogopa kufanya chochote kinachompinga na chochote kinachoenda kinyume na dhamiri yao; hususan wanaogopa kufanya chochote kinachoenda kinyume na mapenzi ya Mungu. Hili tu ndilo laweza kuwa ni kumtambua Mungu. Utafanya nini wazazi wako wakikuzuia kumwamini Mungu? Utampenda vipi Mungu ikiwa mume wako asiye muumini anakutendea mema? Aidha utampendaje Mungu ikiwa ndugu na dada zako wanakuchukia? Ikiwa unamtambua, basi utatenda ipasavyo na kuishi kwa kudhihirisha uhalisi katika hali hizi zote. Ukikosa kutenda wazi na kusema tu kwamba unatambua uwepo wa Mungu, basi wewe ni msemaji tu! Unasema unamwamini na kumtambua. Je, unamtambua kwa njia gani? Unamwamini kwa njia gani? Je, unamwogopa? Unamcha? Unampenda moyoni mwako? Unapokuwa na huzuni bila yeyote wa kuegemea, unahisi Mungu ni wa kupendwa, halafu baadaye unasahau. Huku si kumpenda au kumwamini Mungu! Je, Mungu anataka mwanadamu apate nini mwishoni? Hali zote Nilizozitaja, kama vile: kufikiri kuwa wewe ni mtu mkubwa, kwamba unaelewa mambo upesi, kuwadhibiti wengine, kuwadharau wengine, kuwahukumu watu kwa misingi ya sura zao, kuwadhulumu watu wapole, kutamani pesa za kanisa, na kadhalika—ni wakati tu ambapo tabia hizi zote potovu zimeondolewa kwa kiwango fulani kutoka kwako, ndipo ushindi wako utafanywa dhahiri.

Kazi ya kushinda inayofanywa kwenu nyie ni ya umuhimu mkubwa sana: Kwa upande mmoja, kusudi la hii kazi ni kukikamilisha kikundi cha watu, yaani, kuwakamilisha na kuwa kundi la washindi, kama kundi la kwanza la watu waliofanywa wakamilifu, yaani matunda ya kwanza. Kwa upande wa pili, ni kuruhusu viumbe wa Mungu kufurahia mapenzi ya Mungu, kupokea wokovu mkubwa wa Mungu, na kupokea wokovu kamili wa Mungu, na kumfanya mwanadamu kufurahia si tu huruma na ukarimu wa upendo, ila muhimu zaidi ni kuadibu na hukumu. Tangu uumbaji wa dunia hadi sasa, yote ambayo Mungu amefanya katika kazi Yake ni upendo, bila chuki yoyote kwa mwanadamu. Hata kuadibu na hukumu uliyoiona ni mapenzi pia, upendo wa kweli na wa dhati zaidi; upendo huu huwaongoza wanadamu kwenye njia sahihi ya maisha ya binadamu. Kwa upande wa tatu, ni kushuhudia mbele ya Shetani. Kwa upande wa nne, ni kuweka msingi wa kueneza kazi ya baadaye ya injili. Kazi yote Aliyoifanya ni kumwongoza mwanadamu kwenye njia sahihi ya maisha ya wanadamu, ili kwamba wawe na maisha ya kawaida ya wanadamu, kwani mwanadamu hajui jinsi ya kuishi. Bila uongozi kama

huo, utaishi maisha tupu yasiyo na maana wala thamani, na kamwe hutajua jinsi ya kuwa mwanadamu wa kawaida. Huu ndio umuhimu mkuu wa kumshinda mwanadamu. Nyote ni wa ukoo wa Moabu. Kufanya kazi ya kushinda kwenu ni wokovu wenu mkuu. Nyinyi nyote mnaishi mahala pa dhambi na ufisadi; nyinyi nyote ni watu wapotovu na wenye dhambi. Leo hii hamwezi tu kumwona Mungu, ila la muhimu zaidi, mmepokea kuadibu na hukumu, mmepokea wokovu wa kina, yaani, mmepokea upendo mkubwa zaidi wa Mungu. Yote Ayafanyayo ni mapenzi ya dhati kwako; Hana nia mbaya. Anawahukumu kwa sababu ya dhambi zenu, ili kwamba mweze kujichunguza wenyewe na kupokea wokovu mkubwa. Haya yote hufanywa kwa kusudi la kumkamilisha mwanadamu. Tangu mwanzo hadi mwisho, Mungu amekuwa Akifanya kila Awezalo kumwokoa mwanadamu, na hakika hayuko tayari kuwaangamiza kabisa wanadamu Aliowaumba kwa mikono Yake Mwenyewe. Sasa Amekuja miongoni mwenu kufanya kazi; je, huu si wokovu zaidi? Je, Angalikuchukia, Angaliendelea kufanya kazi ya kiwango hicho cha juu ili kukuongoza wewe Mwenyewe? Ni kwa nini Ateseke hivyo? Mungu hawachukii wala hana nia mbaya juu yenu. Mnapaswa kufahamu kuwa mapenzi ya Mungu ndiyo mapenzi ya kweli zaidi. Anawaokoa kupitia hukumu kwa sababu tu ya uasi wa mwanadamu; la sivyo, hawangepata wokovu. Kwa kuwa hamjui jinsi ya kuishi, na mnaishi katika mahala pa ufisadi na dhambi na ni mapepo wenye ufisadi na uchafu, Hana moyo wa kuwaacha mpotoshwe zaidi; wala Hana moyo wa kutaka kuwaona mkiishi mahala pachafu kama hapa, mkikandamizwa na Shetani apendavyo, Hana moyo wa kuwaacha mtumbukie Kuzimu. Anataka tu kulipata hili kundi lenu na kuwakomboa vilivyo. Hili ndilo kusudi kuu la kufanya kazi ya kushinda miongoni mwenu—ni kwa ajili ya wokovu tu. Iwapo huwezi kuona kuwa kila kitu unachofanyiwa ni mapenzi na wokovu, ukidhani kuwa ni mbinu tu, njia ya kumtesa mwanadamu na kitu kisichoaminika, basi ni bora urudi duniani mwako uendeleo kupata mateso na ugumu wa maisha! Ikiwa uko tayari kuwa kwenye mkondo huu na kufurahia hukumu hii na wokovu huu wa ajabu, na kufurahia baraka hizi ambazo haziwezi kupatikana kokote katika ulimwengu wa wanadamu, na kufurahia upendo huu, basi kuwa mzuri: Salia kwenye mkondo huu ili kukubali kazi ya ushindi ili uweze kufanywa mkamilifu. Leo, unaweza kupitia mateso na usafishaji kidogo kwa sababu ya hukumu ya Mungu, mateso haya ni ya thamani na ya maana. Japo kuadibu na hukumu ni usafishaji na ufichuzi usio na huruma kwa mwanadamu, uliokusudiwa kuadhibu dhambi zake na kuadhibu mwili wake, kazi hii haijanuiwa kukashifu na kuuzima mwili wake. Ufichuzi mkali wa neno ni kwa kusudi la kukuongoza kwenye njia sahihi. Ninyi wenyewe mmeipitia sana kazi hii na ni wazi, haijawaongoza kwenye njia mbaya! Yote ni ili kukufanya uishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida, na yote yanatimizwa na ubinadamu wako wa kawaida. Kila hatua ya kazi hufanywa kwa misingi ya mahitaji yako, kulingana na udhaifu wako, kulingana na kimo chako halisi, na hamjatwikwa mzigo msioweza kuubeba. Japo huwezi kuliona hili wazi kwa sasa, na unajihisi Ninakuwa mgumu kwako, japo unadhani kuwa Ninakuadibu na kukuhukumu

na kukuadibu kila siku kwa kuwa Ninakuchukia, na ingawa unachokipokea ni kuadibu na hukumu, hali halisi ni kuwa yote ni mapenzi kwako, pia ni ulinzi mkubwa kwako. Ikiwa huwezi kung'amua maana ya ndani ya kazi hii, basi huna njia ya kuendelea katika uzoefu wako. Unapaswa kuliwazwa kwa sababu ya huo wokovu. Usikatae kuzirudia busara zako. Baada ya kusafiri umbali huu, unapaswa kuuona wazi umuhimu wa kazi hii ya kushinda. Hupaswi tena kushikilia mtazamo fulani kama huo!

Utendaji (6)

Leo, watu wengi hawawezi kufikia akili alizokuwa nazo Petro—sembuse kuweza kufikia akili alizokuwa nazo Paulo. Hata hawajitambui kama alivyojitambua Paulo. Ingawa Paulo aliangushwa na Bwana kwa sababu alimtesa Bwana Yesu, baadaye alikuwa na azimio la kufanya kazi na kuteseka kwa ajili ya Bwana. Yesu alimpa ugonjwa, na baadaye, Paulo aliendelea kuugua ugonjwa huu mara tu alipoanza kufanya kazi. Kwa nini alisema kuwa alikuwa na mwiba kwenye mwili wake? Kwa kweli, mwiba huo ulikuwa ugonjwa—na kwa Paulo, ulikuwa udhaifu mbaya sana. Haijalishi alifanya kazi kiasi gani au jinsi azimio lake la kuteseka lilivyokuwa kubwa, hakuweza kuondoa mwiba huo. Lakini Paulo alikuwa mwenye ubora mzuri zaidi wa tabia kuliko ninyi watu wa leo, na pia alijitambua na alikuwa na akili nyingi kuwaliko ninyi. Baada ya Paulo kuangushwa na Yesu, aliacha kuwatesa wafuasi wa Yesu, na akaanza kuhubiri na kuteseka kwa ajili ya Yesu. Na ni kitu gani kilichomtia moyo avumilie mateso? Paulo aliamini kwamba, kwa kuwa alikuwa ameuona mwangaza mkuu, ilimlazimu awe na ushuhuda kwa Bwana Yesu, asiwatese tena wafuasi wa Yesu, na asiipinge kazi ya Mungu tena. Paulo alikuwa mmoja wa watu wenye vyeo vya juu katika dini. Alikuwa mwenye maarifa na mwenye vipawa sana, aliwadharau watu wa kawaida, na alikuwa na hulka nzito kuliko watu wengi. Lakini baada ya “mwangaza mkuu” kumwangazia, aliweza kumfanyia Bwana Yesu kazi, akaweka azimio lake kuteseka kwa ajili ya Mungu na kujitoa kwa Mungu, jambo ambalo lilithibitisha kwamba alikuwa na akili. Wakati ambapo alikuwa akiwatesa na kuwakamata wafuasi wa Yesu, Yesu alionekana kwake na kumwambia: “Paulo, mbona wanitesa?” Paulo alianguka chini mara moja na kusema: “Wewe ni nani, Bwana?” Sauti kutoka mbinguni ikasema: “Mimi ndiye Yesu ambaye unamtesa.” Mara moja, Paulo aliamka, na hapo tu ndipo alijua kwamba Yesu alikuwa Kristo, ya kwamba alikuwa Mungu. “Lazima nitii. Mungu amenipa neema hii—nilimtesa hivyo, lakini Hakuniangusha, wala Hakunilaani. Lazima niteseke kwa ajili Yake.” Paulo alitambua kuwa alikuwa amemtesa Bwana Yesu Kristo na sasa alikuwa anawaua wafuasi Wake, kwamba Mungu hakuwa amemlaani, lakini Alikuwa amemwangazia nuru. Hili lilimtia moyo, na akasema: “Ingawa sikuuona uso Wake, niliisikia sauti Yake na nikaona mwangaza Wake mkuu. Ni sasa tu ndipo naona kweli kuwa Mungu ananipenda sana, na kwamba kwa kweli Bwana Yesu Kristo ndiye Mungu anayemhurumia mwanadamu na kuzisamehe

dhambi za wanadamu milele. Ninaona kweli kuwa mimi ni mtenda dhambi.” Ingawa, baadaye, Mungu alitumia vipawa vya Paulo kufanya kazi, lisahau hili kwa sasa. Azimio lake wakati huo, akili yake ya kawaida ya binadamu, na kujitambua kwake—ninyi hamwezi kufanikisha mambo haya. Je, leo hamjapata mwanga mwingi? Je, watu wengi hawajaona kuwa tabia ya Mungu ni ile ya uadhama, ghadhabu, hukumu na kuadibu? Laana, majaribu, na usafishaji vimewapata watu mara nyingi—na wamejifunza nini? Umpata nini kutokana na kufundishwa nidhamu na kushughulikiwa? Maneno makali, mapigo, na hukumu vimekupata mara nyingi, lakini huvitilii maanani. Huna hata akili kidogo aliyokuwa nayo Paulo—je, wewe hujasalia nyuma sana? Pia kulikuwa na mengi ambayo Paulo hakuona kwa dhahiri. Alijua tu kuwa mwangaza ulikuwa umemwangazia, lakini hakujua ya kwamba alikuwa ameangushwa; yeye binafsi aliamini kwamba baada ya mwangaza kumwangazia, lazima ajitumie kwa ajili ya Mungu, ateseke kwa ajili ya Mungu, afanye kila kitu ili amwandalie Bwana Yesu Kristo njia, na awapate watenda dhambi wengi zaidi ili wakombolewe na Bwana. Hili ndilo lilikuwa azimio lake, na kusudi la pekee la kazi yake—lakini alipofanya kazi, ugonjwa huo bado haukumwacha, hadi kifo chake. Paulo alifanya kazi kwa zaidi ya miaka ishirini. Aliteseka sana, na akapitia mateso na dhiki nyingi, ingawa, bila shaka, haya yalikuwa machache sana kuliko majaribu aliyopitia Petro. Je, ni jambo la kusikitishaje ikiwa ninyi hamna hata akili ya Paulo? Hali ikiwa hivi, Mungu anawezaje kuanza kazi kubwa hata zaidi ndani yenu?

Alipokuwa akieneza injili, Paulo alipitia mateso makubwa. Kazi aliyofanya, azimio lake, imani yake, uaminifu, upendo, uvumilivu, na unyenyekevu wake wakati huo, na mambo mengine mengi ya nje aliyoishi kwa kudhihirisha, yalikuwa ya kiwango cha juu kuliko yenu ninyi watu leo. Kusema kwa ukali zaidi, ndani yenu, hakuna akili ya kawaida; hamna hata dhamiri au ubinadamu wowote. Mmepungukiwa na mengi sana! Hivyo, wakati mwingi, hakuna akili ya kawaida na hakuna dalili za kujitambua katika kile mnachoishi kwa kudhihirisha. Ingawa wakati huo Paulo alikuwa akiugua ugonjwa wa mwili, aliendelea kusali na kutafuta: “Ugonjwa huu ni nini kweli? Nimemfanyia Bwana kazi hii yote, kwa nini shida hii hainiachi? Inawezekana kuwa Bwana Yesu ananijaribu? Je, Ameniangusha? Angekuwa ameniangusha, ningekufa wakati huo, na singeweza kumfanyia kazi hii yote, wala singeweza kupokea mwangaza mwingi hivyo. Pia alitambua azimio langu.” Paulo alihisi daima kwamba ugonjwa huu ulikuwa ni Mungu aliyekuwa akimjaribu, kwamba ulikuwa unaichovya imani na utashi wake—hivi ndivyo alivyoona Paulo. Kwa kweli, ugonjwa wake ulikuwa maafu ya ugonjwa yaliyoachwa kutoka wakati ambapo Bwana Yesu alimwangusha. Yalimweka katika shinikizo la hisia, na yakaudhibiti uasi wake. Mkijipata katika hali kama ya Paulo, je, mtafanyaje? Je, azimio na uwezo wenu wa kuteseka unaweza kulingana na ule wa Paulo? Leo, mkikumbwa na ugonjwa fulani, au mpitie jaribio kubwa, na msababishwe kuteseka, ni nani anayejua jinsi mtakavyokuwa. Kama

mngefungiwa kwenye tundu la ndege na mruzukiwe kila mara, mngekuwa sawa. La sivyo mngekuwa tu kama mbwa mwitu, msio na ubinadamu wowote. Kwa hivyo mnapopitia shida au kikwazo kidogo, ni yenye manufaa kwenu; kama lingekuwa jambo rahisi kwenu basi mngeangamia, na kisha mngelindwaje? Leo, ni kwa sababu mnaadibiwa, kuhukumiwa, na kulaaniwa ndiyo mnapewa ulinzi. Ni kwa sababu mmeteseka sana ndiyo mnalindwa. Kama sivyo, mngekuwa tayari mmepotoka. Huku si kufanya mambo yawe magumu kwenu kwa makusudi—asili ya mwanadamu ni ngumu kubadili, na lazima iwe hivyo ili tabia zao zibadilishwe. Leo, hamna hata dhamiri au akili ambazo Paulo alikuwa nazo, wala hamwezi hata kujitambua kama yeye. Lazima mushurutishwe kila wakati, na kila wakati lazima muadibiwe na kuhukumiwa ili roho zenu zichangamshwe. Kuadibu na hukumu ndivyo bora kabisa kwa maisha yenu. Na inapolazimu, lazima pia ukweli unaowafikia uadibiwe; ni hapo tu ndipo mtakapotii kikamilifu. Asili zenu ni kana kwamba bila kuadibu na kulaani, hamngetaka kuinamisha vichwa vyenu, hamngetaka kutii. Bila ukweli ulio mbele yenu, hakungekuwa na matokeo. Ninyi ni duni sana na msio na thamani katika tabia! Bila kuadibu na hukumu, itakuwa vigumu kwenu kushindwa, na itakuwa vigumu kwa udhalimu na kutotii kwenu kushindwa. Asili yenu ya zamani imekita mizizi sana. Kama mngewekwa juu ya kiti cha enzi, hamngefahamu urefu wa mbingu na kina cha dunia, sembuse kujua mnakoelekea. Hamjui hata mlikotoka, hivyo mngewezaje kumjua Bwana wa uumbaji? Bila kuadibiwa na kulaaniwa kwa wakati unaofaa leo, siku yenu ya mwisho ingekuwa imeshawadia kitambo. Hiyo ni kando na majaaliwa yenu—je, hayo hayatakuwa katika hatari ya karibu zaidi? Bila kuadibu na hukumu hii ya wakati unaofaa, ni nani anayejua jinsi ambavyo mngekuwa wenye kiburi, au jinsi ambavyo mngekuwa wapotovu. Kuadibu huku na hukumu hii vimewafikisha leo, na vimehifadhi kuwepo kwenu. Kama bado “mngeelimishwa” kwa kutumia njia zile zile kama za “baba” yenu, ni nani ajuaye mngeingia katika ulimwengu upi! Hamna uwezo wa kujidhibiti na kutafakari kujihusu wenyewe hata kidogo. Kwa watu kama ninyi, mkifuata na kutii tu bila kusababisha ukatizaji au usumbufu wowote, malengo Yangu yatatimia. Je, hamfai kufanya vema zaidi katika kukubali kuadibu na hukumu ya leo? Je, mna chaguo gani jingine? Paulo alipomwona Bwana Yesu akizungumza na kufanya kazi, bado hakuamini. Baadaye, baada ya Bwana Yesu kusulubiwa msalabani na kisha kufufuka, alijua ukweli huu, lakini aliendelea kutesa na kupinga. Hii ndiyo maana ya kutenda dhambi kwa makusudi, na kwa hivyo aliangushwa. Mwanzoni, alijua kwamba kulikuwa na Mfalme kati ya Wayahudi aliyeitwa Yesu, alikuwa amesikia hili. Baadaye, alipokuwa akihubiri hekaluni na kuhubiri nchini kote, alikwenda kinyume na Yesu, akikataa kwa kiburi kumtii mtu yeyote. Vitu hivi vilikuwa kizuizi kikubwa kwa kazi ya wakati huo. Yesu alipokuwa Akifanya kazi, Paulo hakuwatesa na kuwakamata watu moja kwa moja, lakini alitumia mahubiri na maneno kuiharibu kazi ya Yesu. Baadaye, baada ya Bwana Yesu Kristo kusulubiwa msalabani, alianza kuwakamata wafuasi, akikimbia kutoka mahali pamoja hadi pengine na kufanya kila awezalo

kuwatesa. Ni baada tu ya “mwangaza” kumwangazia ndipo alizinduka na kupitia majuto makubwa. Baada ya kuangushwa, ugonjwa wake haukuwahi kumwacha. Wakati mwingine, alihisi kuwa ugonjwa wake ulikuwa umezidi kuwa mbaya, na hakuweza kutoka kitandani. Aliwaza: “Ni nini kinachoendelea? Je, nimeangushwa kweli?” Ugonjwa huo haukuwahi kumwacha, na ni kwa sababu ya ugonjwa huu ndiyo alifanya kazi nyingi. Inaweza kusemwa kwamba Yesu alimwekea Paulo ugonjwa huu kwa sababu ya kiburi chake na ukaidi wake; ilikuwa ni adhabu kwa Paulo, lakini ilifanyika pia ili kutumia vipawa vya Paulo katika kazi ya Mungu, ili kazi Yake iweze kupanuliwa. Kwa kweli, halikuwa kusudi la Mungu kumwokoza Paulo, bali kumtumia. Lakini tabia ya Paulo ilikuwa ya kiburi na ukaidi sana, na kwa hivyo “mwiba” uliwekwa ndani yake. Mwishowe, kufikia wakati ambapo Paulo alimaliza kazi yake, ugonjwa huo haukuwa mateso makubwa sana kwake, na kazi yake ilipokuwa ikiisha, aliweza kusema maneno “Nimepigana vita vizuri, nimeutimiza mwendo wangu, nimeihifadhi imani: Kutoka sasa kuendelea taji la haki limewekwa kwangu”—ambayo alisema kwa sababu hakujua kazi ya Mungu. Kuna wengi kati yenu kama Paulo, lakini kweli mkiwa na azimio la kufuata hadi mwisho wa njia, hamtadhulumiwa. Hatutajadili hapa njia ambazo Paulo alikuwa mwasi na mpinzani; acha tusalie katika sehemu yake ambayo ilikuwa nzuri na yenye kusifika: Alikuwa na dhamiri, na baada ya kupokea “mwangaza” mara moja, aliweza kujitolea kwa Mungu na kuteseka kwa ajili ya Mungu. Hii ilikuwa sifa yake nzuri. Hata hivyo, ikiwa kuna wale ambao wanaamini kwamba kwa sababu alikuwa na sifa nzuri basi alikuwa mtu aliyebarikiwa, ikiwa wanafikiri kwamba hakupasa kuadibiwa, basi haya ni maneno ya watu wasio na akili.

Watu wengi wanapoomba na kusoma maneno ya Mungu, wao husema kuwa wako tayari kumtii Mungu, lakini kisha wanakuwa waasherati faraghani, na wanaona kuwa hilo silo jambo. Maneno ya Mungu yanasemwa tena na tena, yakifichua safu baada ya safu, na ni mpaka tu safu ya chini kabisa ya watu inapofunuliwa ndipo wao “hupata amani” na kuwa wenye kiwango kidogo cha majivuno na ukaidi na wasio na kiburi sana. Hali zenu zikiwa kama zilivyo leo, lazima bado mpigwe kikatili na kufunuliwa, na kuhukumiwa kwa undani kabisa, ili msipate nafasi ya kupumzika. Kwenu, ni bora kuadibu na hukumu kali visiwaache, na shutuma na laana visiwe mbali na ninyi, hili likiwaruhusu muone kwamba mkono wa amri za utawala wa Mungu hauwaachi kamwe. Kama tu katika Enzi ya Sheria, Haruni alipoona ya kuwa Yehova haukuwahi kumwacha (alichokiona kilikuwa mwongozo na ulinzi wa kila wakati wa Yehova; mwongozo wa Mungu mnaouona ninyi leo ni kuadibu, laana, na hukumu), leo pia mkono wa amri za utawala wa Yehova hauwaachi, pia. Hata hivyo, kuna jambo moja ambalo mnaweza kukosa kuwa na wasiwasi kulihusu: Haijalishi jinsi mnavyopinga, kuasi, na kuhukumu, hakutakuwa na madhara yoyote kwa miili yenu. Lakini ikiwa kuna watu wanaovuka mipaka katika upinzani wao na kuizuia kazi, hili halikubaliki; kuna mpaka. Usiyakatize au kuvuruga maisha ya kanisa, na

usiikatize kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa mengine, unaweza kufanya chochote unachotaka. Ukisema hutaki kufuatilia maisha na unatamani kurudi katika ulimwengu, basi harakisha na uende! Mnaweza kufanya chochote mnachotaka mradi hakizuii kazi ya Mungu. Lakini kuna jambo moja zaidi unalohitaji kujua: Mwishowe, watenda dhambi wakaidi kama hao wote wataondolewa. Leo, huenda usikaripiwe, lakini mwishowe, ni sehemu tu ya watu ndio watakaoweza kushuhudia—na wengine wote watakuwa hatarini. Ikiwa hutaki kuwa kwenye mkondo huu, hiyo ni sawa. Watu wa leo hutendewa kwa uvumilivu; Sikuwekei mipaka, mradi huogopi kuadibiwa kesho. Lakini ikiwa uko kwenye mkondo huu, lazima ushuhudie, na lazima uadibiwe. Ikiwa unataka kukataa hili na urudi katika ulimwengu, hiyo ni sawa—hakuna mtu anayekuzuia! Lakini ukifanya kazi inayoharibu na kuvuruga kazi ya Mungu, huwezi kusamehewa kwa ajili ya hilo hata kidogo! Na kuhusu yale ambayo macho yako yanaona na masikio yako kusikia kuhusu ni watu gani wanaoadibiwa, na ni gani ambao familia zao zinalaaniwa—kuna mipaka na vizuizi kwa haya yote. Roho Mtakatifu hafanyi mambo kiholela. Kulingana na dhambi ambazo mmetenda, kama mngetendewa na kuchukuliwa kwa uzito kwa kutegemea udhalimu wenu wenyewe, ni nani kati yenu angeweza kusalia? Ninyi nyote mngepatwa na msiba, na hakuna hata mmoja wenu angekuwa na matokeo mazuri. Lakini leo, watu wengi wanatendewa kwa uvumilivu. Hata ingawa mnahukumu, mnaasi, na kupinga, mradi hamkatizi, basi Nitakutana na ninyi kwa tabasamu. Ikiwa kweli mnafuatilia maisha, basi lazima mwadibiwe kiasi, na lazima mvumilie uchungu wa kutengana na kile mnachopenda ili muende kwenye meza ya upasuaji kufanyiwa upasuaji; lazima ustahimili maumivu, kama tu vile Petro alivyokubali majaribu na mateso. Leo, uko mbele ya kiti cha hukumu. Katika siku zijazo, lazima mwende kwenye “gilotini,” ambao utakuwa wakati ambapo “mnajitoa” wenyewe.

Wakati wa hatua hii ya mwisho ya kazi katika siku za mwisho, labda unaamini kuwa Mungu hatauangamiza mwili wako, na inaweza kusemwa kwamba huenda usipate maradhi yoyote hata ingawa unampinga na kumhukumu Yeye—lakini maneno makali ya Mungu yatakapokujia, wakati uasi na upinzani wako na sura zako mbaya zitakapofunuliwa, hutaweza kujificha. Utajikuta umeshikwa na hofu, usijue la kufanya. Leo, lazima ninyi muwe na dhamiri kiasi. Msichukue nafasi za waovu ambao wanampinga na kumwasi Mungu. Unapaswa kumpa kisogo babu yako wa zamani; hiki ndicho kimo unachopasa kuwa nacho, na huu ndio ubinadamu ambao unapaswa kuwa nao. Wewe daima huwezi kuweka kando matarajio yako ya baadaye au starehe za leo. Mungu anasema: “Mradi mnafanya yote mnayoweza ili kunifuata na kufuatilia ukweli, hakika Nitawafanya muwe wakamilifu. Mara mnapokamilishwa, mtakuwa na hatima nzuri—mtaletwa katika ufalme Wangu ili mfurahie baraka pamoja na Mimi.” Mmeahidiwa hatima nzuri, lakini mahitaji kutoka kwenu hayawezi kupunguzwa kamwe. Pia kuna sharti: Bila kujali kama mtashindwa au kukamilishwa, leo lazima mpitie kuadibu kiasi na mateso kiasi;

lazima mpigwe na kufundishwa nidhamu; lazima msikilize maneno Yangu, mfuata njia Yangu, na mfanye mapenzi ya Mungu—hiki ndicho kile ninyi wanadamu mnapaswa kufanya. Bila kujali jinsi unavyofuatilia, lazima usikie waziwazi hivi. Ikiwa kweli una utambuzi halisi, basi unaweza kuendelea kufuata. Ikiwa unaamini kuwa hakuna matarajio au matumaini hapa, basi unaweza kwenda. Maneno haya yamezungumzwa wazi kwako, lakini ikiwa kweli unatamani kwenda, hili linaonyesha tu kuwa huna dhamiri hata kidogo; hiki kitendo chako kinatosha kuthibitisha kuwa wewe ni pepo. Ingawa unasema unayakabidhi yote katika mipango ya Mungu, kutegemea mwili wako na kile unachoishi kwa kudhihirisha, wewe bado unamilikiwa na Shetani. Ingawa Shetani pia yuko mikononi mwa Mungu, wewe mwenyewe bado ni wa Shetani na bado hujaokolewa kweli na Mungu, kwani wewe bado unaishi chini ya ushawishi wa Shetani. Je, unapaswa kufuatiliaje ili uokolewe? Chaguo ni lako—unapaswa kuchagua njia ambayo unapaswa kuchukua. Mwishowe, kama unaweza kusema: “Sina kitu bora zaidi, ninalipiza upendo wa Mungu kwa dhamiri yangu, na lazima niwe na ubinadamu kidogo. Siwezi kufanikisha chochote kikubwa zaidi, wala ubora wangu wa tabia si mkubwa sana; sielewi maono na maana ya kazi ya Mungu. Mimi hulipiza tu upendo wa Mungu, mimi hufanya chochote ambacho Mungu anataka, na kufanya yote niwezayo. Natekeleza wajibu wangu vizuri kama kiumbe wa Mungu,” kisha nitahisi kuridhika. Huu ni ushuhuda wa juu zaidi ambao unaweza kutoa. Hiki ndicho kiwango cha juu kabisa kinachohitajika kutoka kwa sehemu ya watu: kutekeleza wajibu wa kiumbe wa Mungu. Fanya tu kadiri ya uwezo wako; yanayohitajika kutoka kwako si ya juu sana. Mradi ufanye yote unayoweza kufanya, basi huu ndio ushuhuda wako.

Utendaji (7)

Ubinadamu wenu umepungukiwa sana, mtindo wenu wa maisha ni duni na wa hadhi ya chini sana, hamna ubinadamu, na mumekosa umaizi. Hiyo ndiyo maana mnahitaji kujitayarisha na vitu vya ubinadamu wa kawaida. Kuwa na dhamiri, mantiki na umaizi; kujua jinsi ya kuzungumza na kuyatazama mambo; kuzingatia usafi; kutenda kama binadamu wa kawaida—hizi zote ni sifa za maarifa ya ubinadamu wa kawaida. Mnapotenda kwa njia inayofaa katika vitu hivi, basi mnachukuliwa kuwa na kiwango kinachokubalika cha ubinadamu. Lazima mjitayarishe pia kwa ajili ya maisha ya kiroho. Lazima mjue kazi yote ya Mungu duniani na myapitie maneno Yake. Unapaswa kujua jinsi ya kutii mipango Yake na jinsi ya kutimiza wajibu wa kiumbe aliyeumbwa. Hivi ndivyo vipengele viwili vya kile unachopaswa kukiingia leo—kujitayarisha kwa maisha ya ubinadamu, na kutenda kwa ajili ya maisha ya mambo ya roho. Vyote ni vya lazima.

Watu wengine ni wa upuuzi: Wanajua tu kujipa sifa za ubinadamu. Hakuna kasoro inayoweza kupatikana katika kuonekana kwao; mambo wanayoyasema na njia yao ya

kuzungumza ni ya kufaa, na mavazi yao ni ya heshima na ya kufaa sana. Lakini ni watupu ndani yao; wanaonekana tu kuwa na ubinadamu wa kawaida kwa nje. Kuna wengine wanaolenga tu kile cha kula, kuvaa, na kile cha kusema. Hata kuna wale wanaolenga vitu kama kufagia sakafu, kutandika kitanda na usafi wa jumla pekee. Wanaweza kuwa wamejizoeza vizuri vitu hivi vyote, lakini unapowaomba wazungumze kuhusu maarifa yao ya kazi ya Mungu ya siku za mwisho, ama ya kuadibu na hukumu, ama majaribu na usafishaji, huenda wakaonyesha hawana uzoefu hata kidogo. Unaweza kuwauliza: “Je, una ufahamu wa kazi ya msingi ya Mungu duniani? Je, kazi ya Mungu mwenye mwili leo inatofautiana vipi na kazi ya Yesu? Inatofautiana vipi na kazi ya Yehova? Je, Wao ni Mungu mmoja? Je, Amekuja kutamatisha enzi hii, ama kuwaokoa wanadamu?” Lakini watu kama hawa hawana chochote cha kusema kuhusu masuala haya. Wengine wanajivika mapambo mazuri, lakini ya juujuu: Kina dada wanajivika mapambo mazuri kama maua, na kina ndugu wanavalia kama wana wa wafalme ama wambuji wadogo matajiri. Wanajali tu kuhusu vitu vya nje, kama vitu wanavyokula na kuvalia; ndani yao, wao ni mafukara na hawamfahamu Mungu hata kidogo. Hili lina maana gani? Na kisha kuna wengine wanaovalia kama waombaji maskini—kweli wanaonekana kama watumwa wa Asia Mashariki! Je, kweli hamwelewi Ninachotaka kutoka kwenu? Shirikini kwa karibu: Mmepata nini kweli? Mmemwamini Mungu kwa miaka hii yote, lakini mmevuna hili tu—je, hamna aibu? Je, hamwoni haya? Mmekuwa mkifuatilia kwenye njia ya kweli kwa miaka hii yote, lakini leo kimo chenu bado ni cha chini kuliko cha jurawa! Watazame mabibi wadogo walio miongoni mwenu, warembo kama picha mkiwa mmevalia mavazi na vipodozi vyenu, mkijilinganisha kati yenu—na ni nini mnacholinganisha? Starehe zenu? Matakwa yenu? Je, mnadhani kwamba Nimekuja kuandikisha waonyesha mitindo? Hamna aibu! Maisha yenu yako wapi? Je, kile mnachokifuatilia si tamaa zilizopita kiasi tu? Unadhani kuwa wewe ni mrembo sana, lakini ingawa umevalia kila aina ya umaridadi, kwa kweli wewe si buu anayegaagaa, aliyezaliwa katika rundo la kinyesi? Leo, huna bahati ya kufurahia baraka hizi za mbinguni kwa ajili ya uso wako mrembo, ila kwa sababu Mungu anafanya jambo la kipekee kwa kukuinua. Je, bado huelewi ulikotoka? Maisha yanapotajwa, unafunga mdomo wako na husemi chochote, na unakimya kama sanamu, lakini bado una ujasiri wa kuvalia vizuri! Bado unataka kupaka uso wako rangi nyekundu na poda! Na watazame wambuji walio miongoni mwenu, wanaume waliopotoka wanaoshinda siku kutwa wakitembea huku na kule polepole, wakaidi, na wenye sura tepetevu usoni pao. Je, hivi ndivyo mtu anapaswa kutenda? Je, kila mmoja kati yenu, awe mwamamume ama mwanamke, anazingatia nini siku nzima? Je, mnajua mnamtegemea nani kujilisha? Tazama mavazi yako, tazama kile ulichovuna mikononi mwako, sugua kitambi chako—umefaidika nini kutoka kwa gharama ya damu na jasho ambayo umelipa katika miaka hii yote ya imani? Bado unafikiri kwenda kutalii sehemu maarufu, bado unafikiri kupamba mwili wako unukao—ufuatiliaji usio na maana! Unaombwa uwe mtu wa kawaida, lakini sasa wewe si mtu asiye wa

kawaida tu, wewe ni mpotovu. Mtu kama wewe anawezaje kuwa na ujasiri wa kuja mbele Zangu? Ukiwa na ubinadamu kama huu, ukionyesha uzuri wako na kuringa kwa ajili ya mwili wako, ukiishi daima ndani ya tamaa za mwili—je, wewe si mzao wa mashetani wachafu na pepo waovu? Sitamruhusu shetani mchafu kama huyu aendelee kuishi kwa muda mrefu! Na usifikiri kwamba Sijui kile unachofikiri moyoni mwako. Unaweza kudhibiti vikali tamaa na mwili wako, lakini Naweza kukosa kujua fikira zilizo moyoni mwako? Naweza kukosa kujua tamaa zote za macho yako? Je, ninyi mabibi wadogo hamjirembeshi sana ili kuonyesha miili yenu? Wanaume wana faida gani kwenu? Je, kweli wanaweza kuwaokoa kutoka katika bahari ya mateso? Na kwa wambuji miongoni mwenu, nyote huvalia ili kujifanya muonekane waungwana na wa heshima, lakini, je, hii si hila iliyokusudiwa kuvuta macho kwa sura zenu changamfu? Mnafanya hili kwa sababu ya nani? Wanawake wana faida gani kwenu? Je, wao si chanzo cha dhambi yenu? Enyi wanaume na wanawake, Nimewaambia maneno mengi sana, lakini mmetii machache tu. Masikio yenu hayataki kusikia, macho yenu yamefifia, na mioyo yenu ni migumu kiasi kwamba kuna tamaa tu katika miili yenu, kiasi kwamba mmetegwa nayo, msiweze kutoroka. Ni nani anayetaka kuwakaribia ninyi mabuu, ninyi mnaojifurukuta katika uchafu na masizi? Msisahau kwamba ninyi tu ni wale Niliowatoa kutoka katika rundo la kinyesi, kwamba mwanzoni hamkuwa na ubinadamu wa kawaida. Ninachotaka kutoka kwenu ni ule ubinadamu wa kawaida ambao hamkuwa nao mwanzoni, si kwamba muonyeshe tamaa zenu ama muachilie miili yenu iliyooza, ambayo imeelekezwa na ibilisi kwa miaka mingi sana. Mnapojivisha nguo hivyo, je, hamwogopi kwamba mtategwa kwa kina zaidi? Je, hamjui kwamba mwanzoni mlikuwa wenye dhambi? Je, hamjui kwamba miili yenu imejaa tamaa sana kiasi kwamba hata inavuja kutoka kwa mavazi yenu, ikifichua hali zenu kama mashetani wabaya na wachafu kukithiri? Je, si kweli kwamba mnajua hili vyema zaidi kuliko yeyote mwingine? Mioyo yenu, macho yenu, midomo yenu—je, si vyote vimenajisiwa na mashetani wachafu? Je, hizi sehemu zenu si chafu? Je, unadhani kwamba alimradi hutendi, basi wewe ndiwe mtakatifu kabisa? Je, unadhani kwamba kuvalia mavazi mazuri kunaweza kuficha nafsi zenu duni? Hilo haliwezekani! Nawashauri muwe wenye uhalisi zaidi: Msiwe wadanganyifu na bandia, na msijigambe. Mnaonyeshana tamaa zenu, lakini yote mtakayopata kama malipo ni mateso ya milele na kurudiwa kikatili! Mna haja gani ya kupepeseana macho yenu na kujiingiza katika mapenzi? Je, hiki ndicho kipimo cha uaminifu wenu, kiasi cha uadilifu wenu? Nawachukia kabisa wale miongoni mwenu wanaojihusisha katika uganga na uchawi; Nawachukia sana wale wanaume na wanawake wadogo miongoni mwenu wanaopenda miili yao wenyewe. Ni vyema mjizuie, kwa sababu sasa mnahitajika kuwa na ubinadamu wa kawaida, na hamruhusiwi kuonyesha tamaa zenu—lakini mnachukua kila fursa muwezayo, kwani miili yenu imejaa sana, na tamaa zenu ni kubwa mno!

Kwa nje, maisha yako ya ubinadamu yamepangwa vizuri sana, lakini huna cha kusema unapoambiwa uzungumzie maarifa yako ya maisha; na umepungukiwa sana katika hili. Lazima ujitayarishe na ukweli! Maisha yako ya ubinadamu yamebadilika kuwa bora, na kwa hivyo pia maisha yaliyo ndani yako lazima yabadilike; badili mawazo yako, geuza maoni yako kuhusu imani katika Mungu, badili maarifa na fikira zilizo ndani yako, na ubadili maarifa kumhusu Mungu kama yalivyo ndani ya mawazo yako. Kupitia kushughulikiwa, kupitia ufunuo na ruzuku, badili kwa utaratibu maarifa yako kujihusu, kuhusu maisha ya binadamu, na kuhusu kumwamini Mungu; ufanye ufahamu wako uweze kuwa safi. Kwa njia hii, fikira alizo nazo mwanadamu zinabadilika, jinsi anavyoyaona mambo inabadilika, na mtazamo wake wa kiakili unabadilika. Ni hili tu linaloweza kuitwa mabadiliko katika tabia ya maisha. Huombwi kuyasoma maneno ya Mungu siku nzima ama uoshe nguo na kusafisha. Maisha ya ubinadamu wa kawaida lazima angalau yavumilike kwa kawaida. Aidha, unaposhughulikia masuala ya nje, lazima bado utumie umaizi na mantiki kiasi; lakini kilicho muhimu kabisa ni kwamba ujitayarishe na ukweli wa maisha. Unapojitayarisha kwa ajili ya maisha, lazima ulenge kula na kunywa maneno ya Mungu, lazima uweze kuzungumzia maarifa ya Mungu, maoni yako ya maisha ya binadamu, na hasa, maarifa yako ya kazi iliyofanywa na Mungu wakati wa siku za mwisho. Kwa kuwa unafuatilia uzima, ni lazima ujitayarishe na vitu hivi. Unapokula na kunywa maneno ya Mungu, lazima utathmini uhalisi wa hali yako mwenyewe kulingana na vitu hivi. Yaani, unapogundua dosari zako wakati wa uzoefu wako wa kweli, lazima uweze kupata njia ya kutenda, uweze kupuuza nia na fikira zako zisizo sahihi. Ukijitahidi daima kupata vitu hivi na utake kuvitimiza kwa dhati, basi utakuwa na njia ya kufuata, hutahisi mwenye utupu, na hivyo utaweza kudumisha hali ya kawaida. Ni hapo tu ndipo utakuwa mtu anayebeba mzigo katika maisha yako mwenyewe, aliye na imani. Mbona watu wengine hawawezi kuyaweka maneno ya Mungu katika vitendo baada ya kuyasoma? Je, si kwa sababu hawawezi kuelewa vitu muhimu kabisa? Je, si kwa sababu hawayachukulii maisha kwa uzito? Sasabu ya wao kutoelewa vitu muhimu na kukosa njia ya kutenda ni kuwa wanaposoma maneno ya Mungu, hawawezi kuyahusisha na hali zao wenyewe, wala hawawezi kuwa na ujuzi wa hali zao wenyewe. Watu wengine husema: “Mimi huyasoma maneno ya Mungu na kuyahusisha na hali yangu mwenyewe, na najua kwamba mimi ni mpotovu na mwenye ubora duni wa tabia, lakini siwezi kuyaridhisha mapenzi ya Mungu.” Umeona tu mambo ya nje kabisa; kuna vitu vingi halisi ambavyo huvijui: jinsi ya kuweka kando raha za mwili, jinsi ya kuweka kando kujidai, jinsi ya kujibadili, jinsi ya kuviingia vitu hivi, jinsi ya kuboresha ubora wako wa tabia, na kuanzia kutoka kipengele kipi. Unaelewa tu mambo machache ya nje, na yote unayoyajua ni kwamba kweli umepotoka sana. Unapokutana na ndugu zako, unazungumzia jinsi ulivyopotoka, na inaonekana kwamba unajijua na unabeba mzigo mkubwa kwa ajili ya maisha yako. Kwa kweli, tabia yako potovu haijabadilika, jambo linalothibitisha kwamba hujapata njia ya kutenda. Ikiwa unaongoza kanisa, lazima uweze

kuelewa hali za kina ndugu na kuzionyesha. Je, itatosha kusema tu: “Ninyi watu ni wasiotii na wenye maendeleo kidogo mno!” La, lazima uzungumze hasa kuhusu jinsi kutotii kwao na wao kuwa wenye maendeleo kidogo mno kunavyodhihirishwa. Lazima uzungumzie hali zao za kutotii, mienendo yao ya kutotii, na tabia zao za kishetani, na lazima uyazungumzie mambo haya kwa namna ambayo wanashawishika kabisa kuhusu ukweli katika maneno yako. Tumia mambo ya hakika na mifano kutoa hoja zako, na useme hasa jinsi wanavyoweza kujiondoa kwa tabia ya uasi, na uonyeshe njia ya kutenda—hivi ndivyo jinsi ya kuwashawishi watu. Ni wale tu wanaofanya hivi ndio wanaoweza kuwaongoza wengine; ni wao tu walio na uhalisi wa ukweli.

Sasa mmepewa ukweli mwingi kupitia kufanya ushirika, na lazima uutathmini. Unapaswa kuweza kufikia uamuzi kuhusu kuna ukweli ngapi kwa jumla. Punde unapojua na wewe mwenyewe unaweza kutofautisha kati ya vipengele kadhaa vya ubinadamu wa kawaida ambao mtu anapaswa kuwa nao, vipengele vikuu vya mabadiliko ya tabia ya mtu, kuzidishwa kwa maono, na njia zenye makosa za kujua na kupitia ambazo watu wametumia katika enzi zote—ni hapo tu ndipo utakuwa kwenye njia sahihi. Watu wa dini wanaibudu Biblia kana kwamba ni Mungu; hasa wanazichukulia Injili Nne za Agano Jipya kana kwamba ni nyuso nne tofauti za Yesu na wanazungumzia Utatu wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Haya yote ni ya mzaha kabisa, na nyote mnapaswa kuyabaini; zaidi ya hayo, lazima muwe na maarifa ya kiini cha Mungu aliyepata mwili na kazi ya siku za mwisho. Pia kuna mbinu hizo za kale za kutenda, uongo na mikengeuko hiyo inayohusiana na utendaji—kuishi ndani ya roho, kujazwa na Roho Mtakatifu, kukubali yoyote yatakayokuja, kutii mamlaka—ambayo lazima myajue; mnapaswa kujua jinsi watu walivyotenda awali, na jinsi watu wanavyopaswa kutenda leo. Kuhusu jinsi viongozi na wafanyakazi wanapaswa kushirikiana katika makanisa; jinsi ya kuweka kando kujidai na kujionyesha kuwa bora; jinsi ndugu wanavyopaswa kuishi kwa amani; jinsi ya kuanzisha uhusiano wa kawaida na watu wengine na Mungu; jinsi ya kutimiza ukawaida katika maisha ya binadamu; kile ambacho watu wanapaswa kuwa nacho katika maisha yao ya kiroho; jinsi wanavyopaswa kula na kunywa maneno ya Mungu; ni maneno yapi ya Mungu yanahusiana na maarifa, ni yapi yanayohusu maono, na ni yapi kati yao yanayohusiana na njia ya kutenda—je, haya yote hayajazungumziwa? Maneno haya yako wazi kwa wale wanaofuatilia ukweli, na hakuna mtu anayetendewa kwa upendeleo. Leo, mnapaswa kukuza uwezo wa kuishi kwa kujitegemea, si kutegemea akili ya kutegemeana. Katika siku zijazo, wakati hakuna mtu wa kuwaongoza, mtayafikiria haya maneno Yangu. Katika nyakati za taabu, wakati haiwezekani kuishi maisha ya kanisa, wakati ndugu hawawezi kukutana, wengi wao wakiishi peke yao, wakiweza tu kuwasiliana na watu katika maeneo yao mambo yakiwa mazuri, ni katika nyakati hizi ambapo kwa sababu ya kimo chenu cha sasa, hamwezi kabisa kusimama imara. Wakiwa katikati ya taabu, wengi huona vigumu kusimama imara. Ni wale tu wanaojua njia ya maisha na

wamejitayarisha na ukweli wa kutosha ndio wanaoweza kuendelea kusonga mbele na kufanikisha utakaso na mabadiliko kwa utaratibu. Kupitia taabu si jambo rahisi; ikiwa unafikiri kuwa utazipita kwa siku chache, basi hili linathibitisha jinsi fikira zako zilivyo rahisi! Unafikiri kwamba kwa kuelewa kanuni nyingi, utaweza kusimama imara, lakini hali si hivyo! Ikiwa hufahamu mambo ya maana katika maneno ya Mungu, huwezi kuelewa sifa muhimu za ukweli, na huna njia ya kutenda, basi wakati utakapofika na kitu kikufanyikie, utatumbukia katika vurugu. Hutaweza kuvumilia jaribio la Shetani, wala ujio wa usafishaji. Ikiwa hakuna ukweli ndani yako na huna maono, basi wakati ukifika, hutaweza kujizuia kuanguka. Utakata tamaa kabisa na kusema, “Ni sawa, ikiwa nitakufa liwalo liwe, ni heri niadhibiwe hadi mwisho kabisa! Iwe ni kuadhibiwa ama kurushwa katika ziwa la moto, litimike basi—nitayakabili mambo yanavyonijia!” Mambo yalikuwa hivi wakati wa watendaji huduma: Watu wengine waliamini kwamba walikuwa watendaji huduma kwa vyovyote vile, kwa hivyo hawakufuatilia maisha tena. Walivuta sigara na kunywa pombe, wakafurahisha miili yao, na kufanya kile walichotaka. Wengine walirudi tu duniani kufanya kazi. Mazingira yasiyokalika yako hivi pia; ikiwa huwezi kuyashinda, ukishindwa kujidhibiti hata kidogo, utakata tamaa kabisa. Ikiwa huwezi kushinda ushawishi wa Shetani, utatekwa nyara na Shetani kufumba kufumbua na kuletewa maangamizi tena. Hivyo basi, ni lazima leo ujitayarisha na ukweli; ni lazima uweze kuishi kwa kujitegemea; na unapoyasoma maneno ya Mungu, ni lazima uweze kutafuta njia ya kutenda. Ikiwa hakungekuwa na viongozi ama wafanyakazi wa kukunyunyizia na kukuchunga, unapaswa bado kuweza kupata njia ya kufuata, upate dosari zako mwenyewe, upate ukweli unaopaswa kujitayarisha nao na kutenda. Je, Mungu anaweza kumwandama mwanadamu kila wakati baada ya kuja duniani? Ndani ya fikira zao, watu wengine huamini: “Mungu, usipotufinyanga hadi kwa kiwango fulani, basi kazi Yako haiwezi kuchukuliwa kuwa iliyokamilika, kwa sababu Shetani anakushutumu.” Nakuambia, punde Nitakapomaliza kunena maneno Yangu, basi kazi Yangu itakuwa imekamilika kwa mafanikio. Wakati Sina mengine zaidi ya kusema, basi kazi Yangu itakuwa imekamilika. Mwisho wa kazi Yangu utakuwa thibitisho la kushindwa kwa Shetani, na kwa sababu hiyo, inaweza kusemekana kwamba imemalizwa kwa mafanikio, bila shutuma yoyote kutoka kwa Shetani. Lakini ikiwa bado hakuna mabadiliko ndani yenu wakati kazi Yangu imemalizika, basi watu kama ninyi hamwezi kuokolewa na mtaondolewa. Nitafanya tu kazi inayohitajika. Sitaendelea kazi Yangu duniani hadi ushindwe kwa kiwango fulani, na nyote muwe na maarifa mazuri ya kila kipengele cha ukweli, na ubora wenu wa tabia uboreke na mnishuhudie kwa undani na nje. Hilo halitawezekana! Leo, kazi Nifanyayo ndani yenu inakusudiwa kuwaongoza hadi katika maisha ya ubinadamu wa kawaida; ni kazi ya kukaribisha enzi mpya na ya kuwaongoza wanadamu katika maisha ya enzi mpya. Kazi hii inatekelezwa na kukuzwa miongoni mwenu hatua kwa hatua na moja kwa moja: Nawafunza ana kwa ana; Nawaongoza moja kwa moja; Nawaambia chochote msichokielewa, Nawapa chochote msicho

nacho. Inaweza kusemekana kwamba, kwenu, hii kazi yote ni kwa ajili ya ruzuku yenu ya maisha, kuwaongoza pia katika maisha ya ubinadamu wa kawaida; inakusudiwa hasa kuruzuku maisha ya kundi hili la watu wakati wa siku za mwisho. Kwangu Mimi, hii kazi yote inakusudiwa kukamilisha enzi ya kale na kukaribisha enzi mpya; kumhusu Shetani, Nilipata mwili hasa ili nimshinde. Kazi Nifanyayo miongoni mwenu sasa ni ruzuku yenu ya leo na wokovu wenu wa wakati mzuri, lakini katika miaka hii michache mifupi, Nitawaambia ukweli wote, njia nzima ya maisha, na hata kazi ya siku zijazo; hili litatosha kuwawezesha mpitie mambo kwa njia ya kawaida katika siku zijazo. Nimewaaminia maneno Yangu yote pekee. Sitoi ushawishi mwingine wowote; leo, maneno yote Ninayowazungumzia ni ushawishi Wangu kwenu, kwa sababu leo hamjapitia maneno mengi Ninenayo, na hamwelewi maana yake ya ndani. Siku moja, uzoefu wenu utatimika jinsi tu Nilivyosema leo. Maneno haya ni maono yenu ya leo, na ndiyo mtakayotegemea katika siku zijazo; ni ruzuku ya maisha leo na ushawishi wa siku zijazo, na hakuna ushawishi unaoweza kuwa bora zaidi. Hii ni kwa sababu muda Nilio nao kufanya kazi duniani si mrefu kama muda mlilo nao kupitia maneno Yangu; Namaliza kazi Yangu tu, wakati ninyi mnafuatilia maisha, mchakato unaohusisha safari ndefu katika maisha. Ni baada tu ya kupitia mambo mengi ndipo mtaweza kupata njia ya maisha kikamilifu; ni hapo tu ndipo mtaweza kubaini maana ya ndani ya maneno Nizungumzayo leo. Mtakapokuwa na maneno Yangu mikononi mwenu, wakati kila mmoja wenu amepokea maagizo Yangu yote, punde Nitakapowaagizia yote Nipasayo, na wakati kazi ya maneno Yangu imemalizika, basi utekelezaji wa mapenzi ya Mungu pia utakuwa umetimizwa, bila kujali jinsi matokeo makubwa yamefanikishwa. Siyo jinsi unavyodhani, kwamba ni lazima ubadilishwe hadi kiwango fulani; Mungu hatendi kulingana na fikira zako.

Watu hawakui katika maisha yao kwa siku chache tu. Hata wakila na kunywa maneno ya Mungu kila siku, hili halitoshi. Ni lazima wapitie kipindi cha ukuaji katika maisha yao. Mchakato huu ni muhimu. Kwa sababu ya ubora wa tabia wa watu leo, wanaweza kutimiza nini? Mungu hufanya kazi kulingana na mahitaji ya watu, akitoa matakwa yanayofaa kwa kutegemea ubora wao wa kiasili wa tabia. Iwapo kazi hii ingefanywa miongoni mwa kundi la watu wa ubora wa juu wa tabia: Maneno yaliyotamkwa yangukuwa ya fahari zaidi kuliko yale yaliyotamkwa na ninyi, maono yangukuwa ya fahari zaidi, na ukweli ungekuwa wa fahari zaidi. Maneno mengine yangepasa kuwa makali zaidi, yanayoweza zaidi kuruzuku maisha ya wanadamu, yanayoweza zaidi kufichua siri. Akizungumza miongoni mwa watu kama hawa, Mungu angeruzuku kulingana na mahitaji yao. Matakwa yanayotolewa kwenu leo yanaweza kuitwa ya nguvu zaidi; kazi hii ingefanywa kwa watu wenye ubora wa juu zaidi wa tabia, basi matakwa yangukuwa makubwa zaidi bado. Kazi yote ya Mungu inafanywa kulingana na ubora wa kiasili wa tabia ya watu. Kiwango ambacho watu wamebadilishwa na kushindwa leo ni kiwango cha juu kabisa;

usitumie fikira zako mwenyewe kupima jinsi hatua hii ya kazi imekuwa yenye kufaa. Mnapaswa kuelewa kile mlichio nacho kiasili, na hampaswi kujiona kuwa bora sana. Mwanzoni, hakuna kati yenu aliyefuatilia uzima, ila mlikuwa waombaji wanaozurura mitaani. Kwa Mungu kuwafinyanga hadi kiwango mnachofikiri, kuwafanya nyote mjisujudu sakafuni, mkiwa mmeshawishika kabisa, kana kwamba mmeona maono makubwa—hilo haliwezekani! Haliwezekani kwa sababu yule ambaye hajaona miujiza ya Mungu hawezi kuamini kikamilifu yote Ninayosema. Hata kama mngechunguza maneno Yangu kwa makini, bado hamngeyaamini kikamilifu; hii ndiyo asili ya mwanadamu. Wale wanaofuatilia ukweli watapitia mabadiliko kiasi, ilhali imani ya awali ambayo wale wasiofuatilia ukweli walikuwa nayo itapunguka na hata inaweza kutoweka. Ugumu mkubwa zaidi nanyi ni kwamba hamwezi kuamini kikamilifu bila kuona kutimika kwa maneno ya Mungu, na hamshawishiki bila kuona miujiza Yake. Bila kuona mambo kama haya, ni nani anayeweza kuwa mwaminifu kabisa kwa Mungu? Na kwa hivyo Nasema kwamba kile mnachokiamini si Mungu, ila miujiza. Sasa Nimezungumza waziwazi kuhusu vipengele mbalimbali vya ukweli; kila kipengele ni kamili, na kuna uhusiano wa karibu sana kati ya vipengele vyote. Umeviona, na sasa ni lazima uviweke katika vitendo. Leo Nakuonyesha njia, na katika siku zijazo, unapaswa kuiweka katika vitendo wewe mwenyewe. Maneno Nisemayo sasa yanatoa matakwa kwa watu kutegemea hali zao halisi, na Ninafanya kazi kulingana na mahitaji yao na vitu vilivyo ndani yao. Mungu wa vitendo amekuja duniani kufanya kazi ya vitendo, kufanya kazi kulingana na hali na mahitaji ya kweli ya watu. Yeye anaelewa. Mungu anapotenda, Hawalazimishi watu. Kwa mfano, ufunge ndoa au la linapaswa kutegemea uhalisi wa hali zako; umezungumziwa ukweli kwa uwazi, na Sikuzuii. Familia za watu wengine huwakandamiza ili wasiweze kumwamini Mungu ila wafunge ndoa. Kwa njia hii, ndoa inawafaidi kwa kinyume. Kwa wengine, ndoa haileti manufaa yoyote ila inawagharimu kile walichokuwa nacho awali. Hali yako mwenyewe lazima iamuliwe na mazingira yako ya kweli na azimio lako mwenyewe. Siko hapa ili Nibuni sheria na kanuni Nitakazotumia kutoa matakwa kwenu. Watu wengi kila wakati wanasema kwa sauti, “Mungu ni wa vitendo; kazi Yake inategemezwa kwa uhalisi, na kwa uhalisi wa hali zetu”—lakini unajua kile kinachoifanya hasa iwe ya kweli? Maneno yako matupu yametosha! Kazi ya Mungu ni ya kweli na imetegemezwa kwa uhalisi; haina kanuni ila ni ya bure kabisa, yote ni wazi na isiyofichwa. Maelezo mahususi ya kanuni hizi chache ni yapi? Je, unaweza kusema ni sehemu zipi za kazi ya Mungu ziko hivi? Lazima uzungumze kwa utondoti, lazima uwe na ushuhuda wa aina mbalimbali wa yale uliyoyapitia, na unapaswa kuwa dhahiri kabisa kuhusu sifa hii ya kazi ya Mungu—lazima ujue, na ni hapo tu ndipo utastahili kuzungumza maneno haya. Je, unaweza kujibu mtu akikuuliza: “Mungu mwenye mwili amefanya kazi ipi duniani katika siku za mwisho? Kwa nini unamwita Mungu wa vitendo? ‘Vitendo’ inamaanisha nini hapa? Je, unaweza kuzungumza kuhusu kazi Yake ya vitendo, kuhusu inajumuisha nini hasa? Yesu ni Mungu aliyepata mwili, na Mungu wa

leo pia ni Mungu aliyepata mwili, kwa hivyo tofauti kati Yao ni ipi? Na mifanano ni ipi? Kila mmoja Wao amefanya kazi ipi?” Haya yote yanahusiana na kushuhudia! Usikanganywe kuhusu mambo haya. Kuna wengine wanaosema: “Kazi ya Mungu leo ni ya kweli. Kamwe si onyesho la miujiza na maajabu.” Je, kweli Hatendi miujiza na maajabu? Je, una hakika? Je, unajua kazi Yangu ni gani kweli? Mtu anaweza kusema kwamba Hatendi miujiza na maajabu, lakini si kazi Anayofanya na maneno Anayozungumza yote ni miujiza? Mtu anaweza kusema kwamba Hatendi miujiza na maajabu, lakini hili linategemea jinsi linavyoelezwa na linaelekezwa kwa nani. Bila kuenda kanisani, Amefichua hali za watu, na bila kufanya kazi yoyote kando na kuzungumza, Amewahimiza watu kusonga mbele—je, hii si miujiza? Kwa maneno pekee, Amewashinda watu, na watu wanafuata kwa furaha bila matarajio ama matumaini—je, huu si mwujiza pia? Anapozungumza, maneno Yake yanaibua hali fulani ya moyo ndani ya watu. Ikiwa hawahisi furaha basi wanahisi huzuni; ikiwa hawakabiliwi na usafishaji basi wanakabiliwa na kuadibiwa. Kwa maneno machache makali tu, Anawaadibu watu—je, hili si jambo la mwujiza? Je, wanadamu wanaweza kufanya kitu kama hiki? Umesoma Biblia kwa miaka hii yote, lakini hujaelewa chochote, hujapata umaizi; hukuweza kujitenga na njia hizo za imani zilizopitwa na wakati na za zamani. Huna namna ya kuielewa Biblia. Lakini Yeye anaweza kuielewa Biblia kikamilifu—je, hili si jambo la mwujiza? Ikiwa hakungekuwa na jambo lolote la mwujiza kumhusu Mungu wakati Alipokuja duniani, je, Angeweza kuwashinda? Bila kazi Yake ya ajabu na tukufu, ni nani kati yenu angeshawishika? Machoni pako, inaonekana kana kwamba mtu wa kawaida anafanya kazi na anaishi nanyi—kwa nje, Anaonekana kuwa mtu wa kawaida na wa desturi, unachoona ni sura ya kinafiki ya ubinadamu wa kawaida, lakini kwa kweli, ni uungu unaofanya kazi. Si ubinadamu wa kawaida, ila ni uungu; ni Mungu Mwenyewe anayefanya kazi, kazi Anayofanya kwa kutumia ubinadamu wa kawaida. Kwa hivyo, kazi Yake ni ya kawaida na pia ya mwujiza. Kazi Anayoifanya haiwezi kufanywa na mwanadamu, na kwa kuwa haiwezi kufanywa na watu wa kawaida, inafanywa na kiumbe wa mwujiza. Lakini ni uungu ambao ni wa mwujiza, sio ubinadamu; uungu ni tofauti na ubinadamu. Mtu anayetumiwa na Roho Mtakatifu pia ana ubinadamu wa kawaida na wa desturi, lakini hawezi kufanya kazi hii. Tofauti iko hapa. Unaweza kusema: “Mungu siye Mungu wa mwujiza; Hafanyi chochote cha mwujiza. Mungu wetu anazungumza maneno ambayo ni ya vitendo na halisi. Anakuja kanisani kufanya kazi ya kweli na ya vitendo. Kila siku, Anatuzungumzia ana kwa ana, na Anaonyesha hali zetu ana kwa ana—Mungu wetu ni wa kweli! Anaishi nasi, na kila kitu kumhusu ni cha kawaida kabisa. Hakuna chochote katika sura Yake kinachombainisha kuwa Mungu. Hata kuna nyakati ambapo Anakasirika na tunaona uadhama wa ghadhabu Yake, na wakati mwingine Anatabasamu, na tunaona mwenendo Wake wa kutabasamu. Yeye ni Mungu Mwenyewe aliye na muundo na umbo na, Aliye wa mwili na damu, ambaye ni wa kweli na halisi.” Unaposhuhudia kwa njia hii, ni ushuhuda usio kamili. Utakuwa wa manufaa gani kwa wengine? Ikiwa huwezi kushuhudia

maelezo ya ndani na kiini cha kazi ya Mungu Mwenyewe, basi “ushuhuda” wako ni bure kabisa!

Kumshuhudia Mungu hasa ni suala la kuzungumza kuhusu maarifa yako ya kazi ya Mungu, kuhusu jinsi Mungu huwashinda watu, kuhusu jinsi Yeye huwaokoa watu, kuhusu jinsi Yeye huwabadili watu; ni suala la kuzungumza kuhusu jinsi Yeye huwaongoza watu kuingia katika uhalisi wa ukweli, Akiwawezesha washindwe, wakamilishwe na kuokolewa na Yeye. Kushuhudia kunamaanisha kuzungumza kuhusu kazi Yake na yote ambayo umepitia. Ni kazi Yake pekee inayoweza kumwakilisha, na ni kazi Yake pekee inayoweza kumfichua kwa umma, kwa ukamilifu Wake; kazi Yake inamshuhudia. Kazi na matamshi Yake vinamwakilisha Roho moja kwa moja; kazi Anayofanya inatekelezwa na Roho, na maneno Anayonena yanazungumzwa na Roho. Vitu hivi vinaonyeshwa tu kupitia mwili wa Mungu, lakini kwa kweli, ni maonyesho ya Roho. Kazi yote Anayofanya na maneno yote Anayozungumza yanawakilisha kiini Chake. Ikiwa Mungu hangezungumza ama kufanya kazi baada ya kujivika mwili na kuja miongoni mwa wanadamu, na kisha Awatake mjue uhalisi Wake, ukawaida Wake na kudura Yake, je, ungeweza? Je, ungeweza kujua kiini cha Roho? Je, ungeweza kujua sifa za kiasili za mwili Wake ni zipi? Ni kwa sababu tu mmepitia kila hatua ya kazi Yake ndiyo Anawataka mumshuhudie. Ikiwa hamngekuwa na uzoefu kama huu, basi Hangesisitiza kwamba mumshuhudie. Kwa hivyo, unapomshuhudia Mungu, hushuhudii tu kuhusu sura Yake ya nje ya ubinadamu wa kawaida, lakini pia kazi Anayofanya na njia Anayoongoza; unapaswa kushuhudia kuhusu jinsi ulivyoshindwa na Yeye na umekamilishwa katika vipengele vipi. Unapaswa kuwa na ushuhuda wa aina hii. Ikiwa kila uendapo unasema kwa sauti kubwa: “Mungu wetu amekuja kufanya kazi, na kazi Yake kweli ni ya vitendo! Ametupata bila matendo yasiyo ya kawaida, bila miujiza na maajabu yoyote hata kidogo!” Wengine watauliza: “Unamaanisha nini unaposema kwamba Hafanyi miujiza na maajabu? Anawezaje kuwa Amekushinda bila kufanya miujiza na maajabu?” Na unasema: “Anazungumza na bila kuonyesha miujiza ama maajabu yoyote, Ametushinda. Kazi Yake imetushinda.” Hatimaye, ikiwa huwezi kusema chochote cha maana, ikiwa huwezi kuzungumzia mambo maalum, je, huu ni ushuhuda wa kweli? Mungu mwenye mwili anapowashinda watu, ni maneno Yake ya uungu yanayofanya hivyo. Ubinadamu hauwezi kutimiza hili; silo jambo ambalo mtu yeyote anaweza kutimiza, na hata wale wenye ubora wa juu zaidi wa tabia miongoni mwa watu wa kawaida hawawezi kutimiza hili, kwani uungu Wake ni wa juu zaidi kuliko kiumbe yeyote. Hili ni jambo la ajabu kwa watu; hata hivyo Muumba ni wa juu zaidi kuliko kiumbe yeyote. Viumbe hawawezi kuwa wa juu zaidi kuliko Muumba; ungekuwa wa juu zaidi kumlika, Hangeweza kukushinda, na Anaweza tu kukushinda kwa sababu Yeye ni wa juu zaidi kukuliko. Yeye anayeweza kuwashinda wanadamu wote ndiye Muumba, na hakuna mwingine ila Yeye anayeweza kufanya kazi hii. Maneno haya ni “ushuhuda”—aina ya ushuhuda ambayo unapaswa kuwa nayo. Umepitia kuadibiwa, hukumu,

usafishaji, majaribu, vipingamizi na majaribio hatua kwa hatua, na umeshindwa; umeweka kando matarajio ya mwili, nia zako binafsi, na maslahi ya ndani ya mwili. Yaani, maneno ya Mungu yameushinda moyo wako kabisa. Ingawa hujakua katika maisha yako kwa kiwango Anachotaka, unayajua mambo haya yote na unashawishika kabisa na kile Anachofanya. Kwa hivyo, hili linaweza kuitwa ushuhuda, ushuhuda ambao ni halisi na wa kweli. Kazi ambayo Mungu amekuja kufanya, kazi ya hukumu na kuadibu, inakusudiwa kumshinda mwanadamu, lakini pia Anahitimisha kazi Yake, akimaliza enzi na kutekeleza kazi ya hitimisho. Anakamilisha enzi nzima, Akiwaokoa wanadamu wote, Akiwakomboa wanadamu kutoka katika dhambi kabisa; Anawapata wanadamu Aliowaomba kikamilifu. Unapaswa kushuhudia haya yote. Umepitia kazi nyingi sana ya Mungu, umeiona kwa macho yako mwenyewe na kuipitia wewe binafsi; wakati umefika mwisho kabisa, ni lazima uweze kutenda kazi inayokupasa uifanye. Litakuwa jambo la kusikitisha kweli usipoweza! Katika siku zijazo, wakati injili inaenezwa, unapaswa kuweza kuzungumzia maarifa yako mwenyewe, ushuhudie yote uliyoyapata moyoni mwako na utumie jitihada yote. Kiumbe aliyeumbwa anapaswa kufanikisha hili. Umuhimu wa kweli wa hatua hii ya kazi ya Mungu ni upi? Athari yake ni ipi? Na ni kiwango chake kipi kinatekelezwa ndani ya mwanadamu? Watu wanapaswa kufanya nini? Unapoweza kuzungumza kwa uwazi kuhusu kazi yote ambayo Mungu mwenye mwili amefanya tangu aje duniani, basi ushuhuda wako utakuwa kamili. Unapoweza kuzungumza kwa uwazi kuhusu vitu hivi vitano: umuhimu wa kazi Yake; maudhui yake; kiini chake; tabia inayowakilisha; na kanuni zake, basi hili litathibitisha kwamba unaweza kumshuhudia Mungu, kwamba kweli una maarifa. Mahitaji yangu kwenu si ya juu sana, na yanaweza kutimizwa na wale wote wanaofuatilia kwa kweli. Ikiwa umeazimia kuwa mmoja wa mashahidi wa Mungu, ni lazima uelewe kile Mungu anachochukia sana na kile Mungu Anachopenda. Umepitia kazi Yake nyingi; kupitia kazi hii, ni lazima upate kujua tabia Yake, uelewe mapenzi Yake na mahitaji Yake kwa wanadamu, na utumie maarifa haya kumshuhudia na kutenda wajibu wako. Unaweza tu kusema: “Tunamjua Mungu. Hukumu na kuadibu Kwake havina huruma hata kidogo. Maneno Yake ni makali sana; ni ya haki na uadhama, na hayawezi kukosewa na mtu yeyote,” lakini maneno haya humkimu mwanadamu hatimaye? Yana athari gani kwa watu? Kweli unajua kwamba kazi hii ya hukumu na kuadibu ni ya manufaa zaidi kwako? Hukumu na kuadibu kwa Mungu vinafichua uasi na upotovu wako, sivyo? Vinaweza kutakasa na kuondoa vile vitu vichafu na vipotovu vilimo ndani yako, sivyo? Kusingekuwa na hukumu na kuadibu, hatima yako ingekuwa ipi? Kweli unafahamu kwamba Shetani amekupotosha kwa kiwango cha juu zaidi? Leo, mnapaswa kujitayarisha kwa vitu hivi na mvijue vyema.

Kumwamini Mungu katika nyakati za sasa siyo imani mnayoweza kudhania—kwamba inatosha kuyasoma maneno ya Mungu, kuomba, kuimba, kudansi, kufanya wajibu wenu na

kuishi maisha ya ubinadamu wa kawaida. Kweli imani inaweza kuwa rahisi hivyo? Matokeo ndiyo muhimu. Si idadi ya njia uliyo nayo ya kufanya mambo; badala yake ni jinsi hasa unavyoweza kutimiza matokeo bora zaidi. Unaweza kuyashikilia maneno ya Mungu na kuyaeleza maarifa yako kiasi, lakini unapoyaweka kando, huna chochote cha kusema. Hili linaonyesha kwamba unaweza tu kuzungumzia maandishi na kanuni lakini huna maarifa ya uzoefu. Leo, hutakubalika ukikosa kuelewa kilicho muhimu—hili ni muhimu kabisa kwa kuingia katika uhalisi! Anza kujifunza hivi: Kwanza, yasome maneno ya Mungu, pata kujua vyema maneno ya kiroho yaliyo ndani yake; pata maono muhimu yaliyo ndani yake; tambua sehemu zinazohusu utendaji; viunganishe pamoja vitu hivi, moja baada ya kingine; viingie katikati ya uzoefu wako mwenyewe. Hivi ndivyo vitu muhimu unavyopaswa kuelewa. Utendaji muhimu zaidi wakati wa kula na kunywa maneno ya Mungu ni huu: Baada ya kusoma sura ya maneno ya Mungu, ni lazima uweze kutambua sehemu muhimu zinazohusu maono, na pia ni lazima uweze kutambua sehemu muhimu zinazohusu utendaji; tumia maono kama msingi, na utumie utendaji kama mwongozo wako maishani. Mmepungukiwa na haya zaidi kuliko mengine yote, na ndiyo ugumu wenu mkubwa kabisa; mioyoni mwenu, mnayazingatia kwa nadra. Kwa ujumla, ninyi nyote mpo katika hali ya uvivu, mliokosa motisha, na msiotaka kujitolea ninyi binafsi; ama mnasubiri kwa kukaa tu, na wengine hata hulalamika; hawaelewi nia na umuhimu wa kazi ya Mungu, na ni vigumu kwao kufuatilia ukweli. Watu kama hawa huchukia sana ukweli na hatimaye wataondolewa. Hakuna kati yao anayeweza kukamilishwa, na hakuna anayeweza kusalia. Ikiwa watu hawana azimio kidogo la kupingia nguvu za Shetani, basi hawawezi kuokolewa!

Sasa, iwapo ufuatiliaji wenu umekuwa wa kufaa au la linatathminiwa na kile mlicheo nacho sasa. Hiki ndicho kinachotumiwa kuamua matokeo yenu; yaani, matokeo yenu yanafichuliwa katika kujitolea mlifikofanya na mambo ambayo mmefanya. Matokeo yenu yatadhihirishwa na ufuatiliaji wenu, imani yenu na mambo ambayo mmefanya. Kati yenu nyote, kuna wengi ambao tayari hawawezi kuokolewa, kwani leo ndiyo siku ya kufichua matokeo ya watu, na Sitakanganyikiwa katika kazi Yangu; Sitawaongoza wale wasioweza kuokolewa kabisa katika enzi ifuatayo. Kutakuwa na wakati ambapo kazi Yangu itakuwa imekamilika. Sitafinyanga maiti hizo ambazo haziwezi kuokolewa hata kidogo; sasa ndizo siku za mwisho za wokovu wa mwanadamu, na Sitafanya kazi isiyo ya maana. Usishutumu Mbingu na dunia—mwisho wa dunia unakuja. Hauepukiki. Mambo yamefika hapa, na hakuna kitu ambacho wewe kama mwanadamu unaweza kufanya kuyasimamisha; huwezi kubadili vitu jinsi utakavyo. Jana, hukulipa gharama ya kufuatilia ukweli na hukuwa mwaminifu; leo, wakati umewadia, huwezi kuokolewa; na kesho, utaondolewa, na hakutakuwa na uhuru wa matendo kwa ajili ya wokovu wako. Hata ingawa moyo wangu ni mpole na Ninafanya kila Niwezalo kukuokoa, usipojitahidi

wewe mwenyewe ama kujifikiria hata kidogo, hili linanihusu vipi? Wale wanaofikiria tu miili yao na wanaofurahia faraja, wale wanaoonekana kuamini lakini wasioamini kwa kweli; wale wanaojihusisha katika uganga na uchawi; wale ambao ni wazinzi, walio duni kabisa; wale wanaoiba sadaka za Yehova na mali Yake; wale wanaopenda hongo; wale walio na njozi za kupaa mbinguni; wale ambao ni wenye majivuno na fidhuli, wanaojitahidi tu kwa sababu ya umaarufu na utajiri wa kibinafsi; wale wanaoeneza maneno ya safihi; wale wanaomkufuru Mungu Mwenyewe; wale wanaotoa tu hukumu dhidi ya Mungu Mwenyewe na kumkashifu; wale wanaounda vikundi na kutafuta kujitegemea; wale wanaojitukuza juu ya Mungu, wale wanaume na wanawake wadogo, wa makamo na wakubwa ambao ni wapuuzi na wametegwa katika uasherati; wale wanaume na wanawake wanaofurahia umaarufu na utajiri wa kibinafsi na wanafuatilia hadhi ya kibinafsi miongoni mwa mengine; wale watu wasiotubu walionaswa katika dhambi—je, si wote hawawezi kuokolewa? Uasherati, kutenda dhambi, uganga, uchawi, matusi na maneno ya safihi yote yamejaa kwenu; na ukweli na maneno ya uzima yanakanyagwa miongoni mwenu, na lugha takatifu inachafuliwa miongoni mwenu. Ninyi Mataifa, mliojaa uchafu na uasi! Matokeo yenu ya mwisho yatakuwa yapi? Je, wale wanaopenda mwili, wanaotenda uchawi wa mwili, na waliotegwa katika dhambi ya uasherati wanawezaje kuwa na ujasiri wa kuendelea kuishi! Je, hujui kwamba watu kama ninyi ni mabuu wasioweza kuokolewa? Ni nini kinachowapa haki ya kudai hili na lile? Hadi leo, hakujakuwa na mabadiliko hata kidogo katika wale wasiopenda ukweli na wanapenda tu mwili—watu kama hawa wanawezaje kuokolewa? Wale wasiopenda njia ya uzima, wasiomtukuza Mungu ama kumshuhudia, wanaopanga njama kwa ajili ya hadhi yao wenyewe, wanaojisifu sana—je, si bado wao wako vivyo hivyo, hadi leo? Kuna thamani gani katika kuwaokoa? Iwapo unaweza kuokolewa hakutegemei ukubwa wako ama ni miaka mingapi umekuwa ukifanya kazi, sembuse sifa ambazo umeongeza. Badala yake, kunategemea iwapo ufuatiliaji wako umezaa matunda. Unapaswa kujua kwamba wale waliookolewa ni “miti” inayozaa matunda, siyo miti iliyo na majani yaliyositawi sana na maua mengi lakini ambayo hayazai matunda. Hata kama umeshinda miaka mingi ukizurura mitaani, hilo lina maana gani? Ushuhuda wako uko wapi? Uchaji wako wa Mungu ni kidogo sana kuliko upendo wako kwako mwenyewe na hamu zako zenye tamaa—je, si mtu kama huyu ni mpotovu? Anawezaje kuwa kielelezo na mfano wa wokovu? Asili yako ni isiyorekebisha, wewe ni mwasi sana, huwezi kuokolewa! Je, si watu kama hawa ni wale wataoondolewa? Je, si wakati ambapo kazi Yangu inakamilika ni wakati wa kufika kwa siku yako ya mwisho? Nimefanya kazi nyingi sana na kuzungumza maneno mengi sana miongoni mwenu—kweli mmeyasikiliza kiasi kipi? Mmewahi kutii kiasi kipi? Kazi Yangu ikamilikapo, huo utakuwa wakati ambapo unakoma kunipinga, wakati ambapo unakoma kusimama dhidi Yangu. Nifanyapo kazi, mnanipinga bila kukoma; kamwe hamyatii maneno Yangu. Nafanya kazi Yangu na wewe unafanya “kazi” yako mwenyewe, ukitengeneza ufalme wako mdogo.

Ninyi ni kundi la mbweha na mbwa tu, mnaofanya kila kitu kunipinga! Mnajaribu kila wakati kuwakumbatia wale wanaowapa upendo wao wa dhati—uchaji wenu uko wapi? Kila kitu mfanyacho ni kidanganyifu! Hamna utii wala uchaji, na kila kitu mfanyacho ni kidanganyifu na cha kukufuru! Je, watu kama hawa wanaweza kuokolewa? Wanadamu ambao ni waasherati na wakware daima hutaka kuwavutia makahaba wenye ubembe kwao kwa ajili ya raha zao wenyewe. Sitawaokoa mashetani wa kisherati kama hawa hata kidogo. Nawachukia ninyi mashetani wachafu, na ukware na ubembe wenu utawatumbukiza kuzimuni. Mna nini cha kusema kujihusu? Ninyi mashetani wachafu na pepo waovu ni wa kutia kinyaa! Mnachukiza! Watu ovyo kama ninyi mnawezaje kuokolewa? Je, wale waliotegwa katika dhambi wanaweza kuokolewa bado? Leo, ukweli huu, njia hii, na uzima huu hauwavutii; badala yake mnavutiwa na utendaji dhambi, fedha, hadhi, umaarufu na faida; mnavutiwa na raha za mwili; sura nzuri za wanaume na uzuri wa wanawake. Ni nini kinachowastahiki kuingia katika ufalme Wangu? Sura yenu hata ni ya juu zaidi kuliko ya Mungu, hadhi yenu hata ni ya juu kuliko ya Mungu sembuse fahari yenu kubwa miongoni mwa wanadamu—mmekuwa sanamu ambayo watu wanaabudu. Je, hujageuka kuwa malaika mkuu? Wakati matokeo ya watu yanafichuliwa, ambao pia ndio wakati kazi ya wokovu itakaribia kuisha, wengi kati yenu mtakuwa maiti msioweza kuokolewa na lazima muondolewe. Wakati wa kazi ya wokovu, Mimi ni mwenye huruma na mzuri kwa watu wote. Kazi inapokamilika, matokeo ya watu wa aina tofauti yatafichuliwa, na wakati huo, Sitakuwa mwenye huruma na mzuri tena, kwa kuwa matokeo ya watu yatakuwa yamefichuliwa, na kila mmoja atakuwa amesainishwa kulingana na aina yake, na hakutakuwa na haja ya kufanya kazi zaidi ya wokovu, kwa sababu enzi ya wokovu itakuwa imepita, na kwa sababu imepita, haitarudi.

Utendaji (8)

Ninyi bado hamwelewi vipengele mbalimbali vya ukweli, na bado kuna makosa machache na mikengeuko katika kutenda kwenu; katika mambo mengi mnaishi kulingana na fikira na mawazo yenu, kamwe msiweze kuelewa kanuni za utendaji. Hivyo, bado ni muhimu kuwaongoza watu kuingia kwenye njia sahihi; kwa maneno mengine, ili waweze kudhibiti maisha yao ya binadamu na ya kiroho, waweke vipengele hivyo viwili katika vitendo, na ili kwamba wasihitaji kusaidiwa ama kuelekezwa mara kwa mara. Ni hapo tu ndipo watakapokuwa na kimo cha kweli. Na hata ikiwa hakuna mtu wa kukuelekeza katika siku zijazo, bado utaweza kujipatia uzoefu mwenyewe. Leo, ukielewa ni vipengele vipi vya ukweli ndivyo muhimu na ni vipi visivyo muhimu, katika siku zijazo, utaweza kuingia katika uhalisi. Leo, ninyi mnaelekezwa kwenye njia sahihi, hili likiwaruhusu muelewe ukweli mwingi, na katika siku zijazo mtaweza kuendelea kwa kina zaidi. Inaweza kusemwa kuwa kile ambacho watu wanafanywa kuelewa sasa ni njia safi kabisa. Leo, unapelekwa kwenye njia sahihi—na siku moja, wakati ambapo

hakuna mtu yeyote wa kukuelekeza, utatenda na kusonga mbele kwa kina zaidi kulingana na njia hii iliyo safi zaidi kuliko zote. Leo, watu wanafanywa kuelewa ni vitendo vya aina gani ndivyo sahihi na ni vya aina gani vilivyopotoka. Baada ya kuelewa mambo haya, katika siku zijazo, uzoefu wao utakuwa wa kina zaidi. Leo, fikira, mawazo na upotovu katika kutenda kwenu vinageuzwa, na njia ya kutenda na kuingia inafunuliwa kwenu, na baada ya hapo hatua hii ya kazi itakamilika, na ninyi mtaanza kuitembea njia ambayo ninyi wanadamu mnapaswa kuitembea. Kisha, kazi Yangu itakuwa imekamilika, na kutoka wakati huo kuendelea hamtakutana na Mimi tena. Leo, kimo chenu bado ni kidogo. Kuna shida nyingi ambazo hutokana na asili na kiini cha mwanadamu, na kwa hivyo pia, kuna mambo fulani yaliyokita mizizi ambayo bado hayajafukuliwa. Hamwelewi maelezo ya ndani ya kiini na asili ya watu, na bado mnahitaji Mimi niyaonyeshe, la sivyoyote hamtaweza kuyatambua. Wakati fulani ambapo mambo yaliyo ndani yenu kabisa yamefunuliwa, haya ndiyo yanayojulikana kama kuadibu na hukumu. Ni wakati tu ambapo kazi Yangu imetekelezwa kabisa na kwa ukamilifu ndipo Nitakapoitamatisha. Kadiri viini vyenu potovu vinavyofunuliwa kwa kina zaidi, ndivyo mtakavyokuwa na maarifa zaidi, na hili litakuwa jambo lenye umuhimu mkubwa kwa ushuhuda na kukamilishwa kwenu kwa baadaye. Ni wakati tu ambapo kazi ya kuadibu na hukumu itakapokuwa imetekelezwa kabisa ndipo kazi Yangu itakuwa imekamilika, na nyinyi mtanijua kutokana na kuadibu na hukumu Yangu. Hamtajua tabia na haki Yangu tu, lakini la muhimu zaidi, mtajua kuadibu na hukumu Yangu. Wengi kati yenu wana mawazo makubwa juu ya upya na kiwango cha maelezo ya kazi Yangu. Bila kujali hayo, mnapaswa kuona kwamba kazi Yangu ni mpya na yenye maelezo mengi, na kwamba Ninawafundisha kutenda uso kwa uso, Nikiwashika kwa mkono. Hili tu ndilo lenye faida kwa utendaji wenu na kwa uwezo wenu wa kusimama imara katika siku zijazo; la sivyoyote, mngekuwa kama majani ya msimu wa kupukutika kwa majani, yaliyonyauka, ya manjano na yaliyokauka, bila hata chembe ya thamani. Mnapaswa kujua kuwa Ninajua kila kitu kilicho ndani ya mioyo na roho zenu; na mnapaswa kujua kuwa kazi Ninayofanya na maneno Ninayonena ni yenye werevu na maana iliyofichika sana. Kwa kutegemea tabia na ubora wenu wa tabia, hivi ndivyo mnavyopaswa kushughulikiwa. Ni kwa njia hii tu ndiyo maarifa yenu kuhusu kuadibu na kuhukumu Kwangu yanaonekana wazi zaidi, na hata ikiwa hujui leo, kesho utajua. Kiumbe yeyote aliyeumbwa ataanguka kati ya maneno Yangu ya kuadibu na hukumu, kwa maana Mimi sivumilii upinzani wa mtu yeyote Kwangu.

Ninyi nyote lazima muweze kuyadhibiti maisha yenu kwa busara. Unaweza kupanga kila siku kwa namna yoyote unayotaka; una uhuru kufanya chochote upendacho; unaweza kusoma maneno ya Mungu, usikilize nyimbo au mahubiri, au kuandika maelezo ya ibada; na ikiwa inakupendeza, unaweza kuandika nyimbo. Je, vyote hivi havijumuishi maisha mazuri? Hivi vyote ni vitu vinavyopaswa kuunda maisha ya mwanadamu. Watu wanapaswa kuishi kwa

kawaida; ni wakati tu ambapo wamevuna matunda katika ubinadamu wao wa kawaida na katika maisha yao ya kiroho ndipo wanaweza kuzingatiwa kuwa wameingia katika maisha yanayofaa. Leo, sio tu katika ubinadamu ndiyo unakosa utambuzi na mantiki. Pia kuna maono mengi ambayo yanafaa kujulikana ambayo watu lazima wajiandae nayo, na bila kujali funzo lolote unalokabiliwa nalo, hilo ndilo funzo unalopaswa kujifunza; lazima uweze kuzoea mazingira. Kuboresha kiwango chako cha elimu lazima kufanyike kwa muda mrefu ili kuweze kuzaa matunda. Kuna vitu fulani ambavyo lazima ujiandae navyo ili uwe na maisha yanayofaa ya kibinadamu, na lazima pia uelewe kuingia kwako katika maisha. Leo, umepata kuelewa maneno mengi ya Mungu—kwa kuyasoma tena sasa—ambayo hukuelewa wakati huo, na moyo wako umeimarika zaidi. Haya pia ndiyo matokeo ambayo umepata. Katika siku yoyote ulapo na kunywa maneno ya Mungu na kuna ufahamu kiasi ndani yako, unaweza kuwasiliana kwa karibu na ndugu zako kwa uhuru. Je, haya siyo maisha unayopaswa kuishi? Wakati mwingine, maswali kadhaa huibuliwa, au unatafakari mada fulani, na inakufanya uwe bora zaidi katika kutambua, na inakupua umaizi na busara zaidi, ikikuruhusu uelewe ukweli fulani—na hiki sicho kile kilicho ndani ya maisha ya kiroho yanayozungumziwa leo? Haikubaliki kuweka tu kipengele kimoja cha maisha ya kiroho katika vitendo; kula na kunywa maneno ya Mungu, kuomba, na kuimba nyimbo vyote vinajumuisha maisha ya kiroho, na unapokuwa na maisha ya kiroho, lazima pia uwe na maisha yenye ubinadamu unaofaa. Leo, mengi ya yale yanayosemwa ni kwa ajili ya kuwapa watu mantiki na umaizi, kuwaruhusu wamiliki maisha ya ubinadamu unaofaa. Maana halisi ya kuwa na umaizi; maana halisi ya kuwa na mahusiano yanayofaa kati ya watu wawili; jinsi unavyopaswa kuingiliana na watu—unapaswa kujiandaa na vitu hivi kupitia kula na kunywa maneno ya Mungu, na kile kinachohitajika kutoka kwako kinapatikana kupitia ubinadamu wa kawaida. Jiandae na vitu ambavyo unapaswa kujiandaa navyo, na usizidi kile kinachofaa; watu wengine hutumia maneno na misamiati ya kila aina, na katika hili wanaonyesha uzuri wao. Na kuna wengine ambao husoma vitabu vya kila aina, ambapo wanaendekeza tamaa za mwili. Wao hata huchunguza na kuiga wasifu na nukuu za wale wanaodaiwa kuwa watu maarufu wa ulimwengu, na wanasoma vitabu vya ponografia—hili ni jambo la kuchekeza hata zaidi! Watu kama hawa hawajui njia ya kuingia katika maisha, sembuse kujua kazi ya Mungu leo. Hawajui hata jinsi ya kushinda kila siku. Maisha yao ni matupu hivi! Wao hawajui kabisa kile wanachopaswa kuingia katika. Kile wanachofanya ni kuzungumza na kuwasiliana na wengine, kana kwamba kuzungumza kunakuwa mbadala wa kuingia kwao wenyewe. Je, hawana aibu? Hawa ni watu wasiojua jinsi ya kuishi, na wasioelewa maisha ya binadamu; wao hushinda siku nzima wakila kupita kiasi, na kufanya vitu visivyo vya maana—kuna maana gani ya kuishi kwa namna hii? Nimeona kuwa kwa watu wengi, mbali na kufanya kazi, kula, na kuvaa, wakati wao wa thamani unatumika kwa vitu visivyo vya maana, iwe ni kufanya mzaha na kucheza, kufanya umbeya, au kulala siku nzima. Je, haya ni maisha ya

mtakatifu? Je, haya ni maisha ya mtu anayefaa? Je, maisha kama haya yanaweza kukufanya uwe mkamilifu wakati ambapo ni duni, yaliyo nyuma kimaendeleo na yasiyojali? Je, uko tayari sana kujitolea kwa Shetani bure? Wakati maisha ya watu ni rahisi, na hakuna mateso katika mazingira yao, hawawezi kupata uzoefu. Katika mazingira matulivu, ni rahisi kwa watu kuharibika tabia—lakini mazingira magumu hukufanya uombe kwa dharura zaidi, na kufanya hali iwe kwamba huwezi kuthubutu kumwacha Mungu. Kadiri maisha ya watu yalivyo rahisi na yasiyo na furaha zaidi, ndivyo wanavyohisi zaidi kuwa hakuna sababu ya kuishi, na hata wanahisi kuwa ni bora wafe. Hivi ndivyo jinsi miili ya watu wapotovu ilivyo; wao hufaidika tu wakikabiliwa na majaribu.

Hatua hiyo ya kazi ya Yesu ilifanywa huko Yudea na Galilaya, na watu wasio Wayahudi hawakujua kuihusu. Kazi Aliyofanya ilikuwa ya siri sana, na hakuna mataifa mengine mbali na Israeli yaliyojua kuihusu. Ni wakati tu ambapo Yesu alimaliza kazi Yake na ikasababisha vurugu ndipo watu walijua kuihusu, na wakati huo Alikuwa ameondoka. Yesu alikuja kufanya hatua moja ya kazi, Akapata watu kiasi, na Akakamilisha hatua ya kazi. Katika hatua yoyote ya kazi ambayo Mungu hufanya, kuna wengi wanaomfuata. Kama ingetokelezwa na Mungu Mwenyewe pekee yake, haingekuwa na maana; lazima kuwe na watu wa kumfuata Mungu mpaka Atekeleze hatua hiyo ya kazi hadi mwisho kabisa. Ni wakati tu ambapo kazi ya Mungu Mwenyewe imekamiliika ndipo watu huanza kutekeleza kazi iliyoagizwa na Mungu, na hapo tu ndipo kazi ya Mungu huanza kuenea. Mungu hufanya tu kazi ya kuikaribisha enzi mpya; kazi ya watu ni kuiendeleza. Kwa hivyo, kazi ya leo haitadumu kwa muda mrefu; maisha Yangu na mwanadamu hayataendelea kwa muda mrefu sana. Ninakamilisha kazi Yangu tu, na kuwaacha ninyi mtekeleze wajibu mnaopaswa kutekeleza, ili kazi hii na injili hii iweze kuenea haraka iwezekanavyo kati ya wasio Wayahudi na nchi nyingine—ni hivyo tu ndivyo mnavyoweza kutimiza wajibu wenu kama wanadamu. Wakati wa sasa ndio muhimu zaidi ya nyakati zote. Ukiupuuza, wewe ni mpumbavu; ukila na kunywa maneno haya na kupitia kazi hii katika mazingira haya, na bado unakosa azimio la kufuatilia ukweli, na hufahamu hata kidogo mzigo—siku zako za baadaye zitakuwaje? Je, mtu kama wewe hastahili kuondolewa?

Hudumu Jinsi Waisraeli Walivyohudumu

Siku hizi, watu wengi hawatilii maanani ni mafunzo yapi wanayopaswa kupata wakati wanaposhirikiana na wengine. Nimegundua kwamba wengi wenu hawawezi kupata mafunzo hata kidogo wakati wanaposhirikiana na wengine; wengi wenu huyashikilia maoni yenu wenyewe. Unapofanya kazi kanisani, unatoa maoni yako na mtu mwingine anatoa yake, na maoni hayo hayana uhusiano; kwa kweli hamshirikiani hata kidogo. Ninyi nyote mnajishughulisha sana na kuwasiliana tu kuhusu utambuzi wenu wenyewe ama kuachilia

“mizigo” mliyoibeba ndani yenu, bila kutafuta uzima kwa namna yoyote ile. Unaonekana kufanya kazi kwa njia ya uzembe tu, daima ukiamini kwamba unapaswa kuitembea njia yako mwenyewe bila kujali kile ambacho mtu mwingine anasema ama kufanya; unafikiria kwamba unapaswa kushiriki jinsi Roho Mtakatifu anavyokuongoza, bila kujali hali za wengine zinaweza kuwa zipi. Hamwezi kugundua uwezo wa wengine, na wala hamwezi kujichunguza. Kukubali kwenu mambo kumepotoka na kuna makosa sana. Inaweza kusemwa kwamba hata sasa bado mnaonyesha unyoofu mwingi, kana kwamba mmerudia ugonjwa huo wa zamani. Kwa mfano, hamwasiliani kwa njia inayofanikisha uwazi kamili, kwa mfano, kuhusu aina ya matokeo ambayo mmepata kutoka kwa kazi katika makanisa fulani, ama kuhusu hali zako za ndani za siku hizi na kadhalika; kamwe hamwasiliani hata kidogo kuhusu mambo kama hayo. Hamshiriki hata kidogo katika vitendo kama kuyaacha mawazo yenu wenyewe ama kujikana. Viongozi na wafanyakazi wanafikiri tu kuhusu jinsi ya kuwazuia ndugu zao wasiwe hasi na jinsi ya kuwafanya waweze kufuata kwa juhudi. Hata hivyo, ninyi nyote mnafikiri kwamba kufuata kwa juhudi pekee kunatosha, na kimsingi, hamwelewi maana ya kujijua na kujikana, sembuse kuelewa maana ya kuhudumu kwa kushirikiana na wengine. Mnafikiri tu kuhusu ninyi wenyewe kuwa na nia ya kuulipiza upendo wa Mungu, kuhusu ninyi wenyewe kutaka kuishi kwa kudhihirisha mtindo wa Petro. Hamfikirii kuhusu kitu kingine isipokuwa mambo haya. Hata unasema kwamba bila kujali yale watu wengine wanayofanya, hutatii bila kufikiria, na kwamba bila kujali jinsi watu wengine walivyo, wewe mwenyewe utatafuta kukamilishwa na Mungu, na hiyo itatosha. Hata hivyo, ukweli ni kwamba kutaka kwako hakujapata maonyesho thabiti kwa kweli. Je, haya yote sio mwenendo ambao mnadhihirisha siku hizi? Kila mmoja wenu anashikilia utambuzi wake mwenyewe, na nyote mnatamani kukamilishwa. Naona kwamba mmehudumu kwa muda mrefu sana bila kufanya maendeleo mengi; hasa katika funzo hili la kufanya kazi pamoja kwa upatanifu, hamjafanikisha chochote hata kidogo! Unapokwenda katika makanisa unawasiliana kwa njia yako, na wengine wanawasiliana kwa njia zao. Ushirikiano wa upatanifu unafanyika mara chache sana, na hili ni kweli hata zaidi kwa wafuasi walio chini yako. Yaani, ni mara chache ambapo yeyote kati yenu anaelewa maana ya kumhudumia Mungu, ama jinsi mtu anavyopaswa kumhudumia Mungu. Mmekanganyikiwa na mnayachukulia mafunzo ya aina hii kama mambo madogo. Hata kuna watu wengi ambao hawakosi kutenda kipengele hiki cha ukweli tu, lakini ambao pia wanafanya makosa kwa makusudi. Hata wale ambao wamehudumu kwa miaka mingi wanapigana na kupangiana njama nao ni wenye wivu na wenye kupenda kushindana; ni kila mtu na wake, na hawashirikiani hata kidogo. Je, mambo haya yote hayawakilishi kimo chenu cha kweli? Ninyi watu mnaohudumu pamoja kila siku ni kama Waisraeli, ambao kila siku walimhudumia Mungu Mwenyewe moja kwa moja hekaluni. Inawezekanaje kwamba ninyi watu, mnaomhudumia Mungu, hamjui jinsi ya kushirikiana ama jinsi ya kuhudumu?

Wakati huo, Waisraeli walimhudumia Yehova moja kwa moja hekaluni, na walikuwa na utambulisho wa makuhani. (Bila shaka, si kila mtu alikuwa kuhani; ni baadhi tu ya waliomhudumia Yehova hekaluni ndio waliokuwa na utambulisho huo.) Walijitwika mataji waliyopewa na Yehova (kumaanisha kwamba walitengeneza mataji haya kulingana na matakwa ya Yehova; sio kwamba Yehova aliwapa mataji haya moja kwa moja). Pia walivalia majoho ya ukuhani waliyopewa na Yehova na kumhudumia moja kwa moja hekaluni kutoka asubuhi hadi usiku wakiwa pekupeku. Huduma yao kwa Yehova haikuwa ya ovyo ovyo hata kidogo, na haikuhusisha kuharakisha huku na kule bila kufikiria; badala yake, yote ilifanywa kulingana na sheria ambazo hazingekiukwa na yeyote aliyemhudumia moja kwa moja. Wote walilazimika kufuata kanuni hizi; vinginevyo, wangepigwa marufuku kuingia hekaluni. Iwapo yeyote kati yao angevunja sheria za hekalu—yaani, iwapo yeyote angeasi amri za Yehova—basi ingebidi mtu huyo atendewe kulingana na sheria ambazo Alikuwa ametoa, na hakuna mtu aliyeruhusiwa kupinga jambo hili ama kumlinda huyo mvunja sheria. Bila kujali walikuwa wamemhudumia Mungu kwa miaka mingapi, wote walihitajika kufuata sheria. Kwa sababu hii, makuhani wengi sana walivalia majoho ya ukuhani na kumhudumia Yehova bila kusita kwa njia hii mwaka mzima, hata ingawa hakuwa Amewatendea kwa njia yoyote ya kipekee. Hata waliishi maisha yao yote mbele ya madhabahu na hekaluni. Hili lilikuwa onyesho la uaminifu na utii wao. Si ajabu kwamba Yehova aliwapa baraka kama hizo; ilikuwa ni kwa sababu tu ya uaminifu wao ndipo walipokea fadhila na kuyaona matendo yote ya Yehova. Wakati huo, Yehova alipofanya kazi huko Israeli kati ya wateule Wake, aliwatolea madai makali sana. Wote walikuwa watiifu sana na wakazuiliwa na sheria hizi; sheria hizi zilitumika kulinda uwezo wao wa kumcha Yehova. Hizi zote zilikuwa amri za utawala za Yehova. Iwapo kuhani yeyote kati yao hakuishika Sabato ama kukiuka amri za Yehova, na iwapo angegunduliwa na watu wa kawaida, basi mtu huyo angebebwa mara moja hadi mbele ya madhabahu na kupigwa mawe hadi afe. Maiti hizo hazikuruhusiwa kuwekwa ndani ama karibu na hekalu; Yehova hakuruhusu jambo hilo. Yeyote ambaye angefanya hivyo angechukuliwa kuwa mtu aliyetoa “dhabihu zenye kukufuru,” na angerushwa ndani ya shimo kubwa na kuuawa. Bila shaka, watu wote kama hao wangepoteza maisha yao; hakuna yeyote ambaye angesamehewa. Hata kuna wale ambao walitoa “moto wenye kukufuru”: yaani, watu ambao hawakutoa dhabihu katika siku zilizotengwa na Yehova wangechomwa na moto Wake pamoja na vitu vyao vya kutolewa dhabihu, ambavyo havikuruhusiwa kubaki kwenye madhabahu. Matakwa yaliyotolewa kwa makuhani yalikuwa kama ifuatavyo: Hawakuruhusiwa kuingia hekaluni, ama hata kwenye uwanja wake wa nje bila kuosha miguu yao kwanza; wangeingia hekaluni tu iwapo wangukuwa wamevalia majoho yao ya ukuhani; wangeingia hekaluni tu iwapo wangukuwa wamejitwika mataji yao ya ukuhani; hawangeingia hekaluni iwapo wangukuwa wamechafuliwa na maiti; hawangeingia hekaluni baada ya kugusa mkono wa mtu dhalimu, isipokuwa kama wangenawa mikono yao kwanza; na

hawangeingia hekaluni baada ya kujitia unajisi na wanawake (kwa miezi mitatu, si milele), wala hawakuruhusiwa kuuona uso wa Yehova. Muda ulipopita—kumaanisha kwamba baada ya miezi mitatu tu ndipo wangeruhusiwa kuvalia majoho masafi ya ukuhani—kisha walilazimika kuhudumu katika uwanja wa nje kwa siku saba kabla ya kuweza kuingia hekaluni ili kuuona uso wa Yehova. Waliruhusiwa kuvalia haya mavazi yoyote ya ukuhani ndani ya hekalu tu, wala si nje kamwe, ili kuepuka kulinajisi hekalu la Yehova. Iliwabidi wale wote ambao walikuwa makuhani kuwaleta wahalifu ambao walikuwa wamekiuka sheria za Yehova mbele ya madhabahu Yake, ambapo wanguuwa na watu wa kawaida; vinginevyo, moto ungemtekeleza kuhani ambaye alikuwa ameshuhudia uhalifu huo. Kwa hivyo, walikuwa waaminifu daima kwa Yehova, kwa sababu sheria Zake zilikuwa kali sana kwao, na kamwe hawangethubutu hata kidogo kukiuka amri Zake za utawala kiholela. Waisraeli walikuwa waaminifu kwa Yehova kwa sababu walikuwa wameuona mwale Wake, na walikuwa wameuona mkono Alioutumia kuwaadibu watu, na pia kwa sababu mwanzoni walikuwa wamemcha sana. Kwa hivyo, walichokipata hakikuwa tu mwale wa Yehova, bali utunzaji, ulinzi na baraka Zake. Uaminifu wao ulikuwa kwamba walifuata maneno ya Yehova katika matendo yao yote, na hakuna mtu aliyeasi. Iwapo uasi wowote ungetokea, wale wengine bado wangetekeleza maneno ya Yehova, wakimuua yeyote aliyempinga Yehova, na kutomficha mtu huyo kutoka kwa Yehova hata kidogo. Wale walioikiuka Sabato, waliokuwa na hatia ya uzinzi, na wale walioiba dhabihu zilizotolewa kwa Yehova wangedhibiwa vikali hasa. Wale walioikiuka Sabato walipigwa mawe hadi wakafa na wao (watu wa kawaida), ama walipigwa mijeledi hadi kufa, bila yeyote kusamehewa. Wale wote waliotenda uzinzi—hata wale waliotamani wanawake warembo ama walioibua fikira za uasherati baada ya kuwaona wanawake waovu, ama walioshikwa na tamaa walipowaona wanawake vijana—wote wanguuwa. Iwapo mwanamke yeyote kijana ambaye hakujifunika ama kuvalia shela angemshawishi mwanaume kufanya kitendo haramu, mwanamke huyo angeuawa. Ikiwa mwanamume huyo aliyekiuka sheria za aina hii alikuwa kuhani (mtu aliyehudumu hekaluni), angesulubiwa ama kunyongwa. Hakuna mtu kama huyo angeruhusiwa kuishi, na hakuna hata mmoja kati yao angefadhiwa na Yehova. Jamaa za mtu kama huyu hawangeruhusiwa kumtolea Yehova dhabihu mbele za madhabahu kwa miaka mitatu baada ya kifo chake, wala hawangeruhusiwa kushiriki katika dhabihu ambazo Yehova aliwapa watu wa kawaida. Wangeweza kuweka ng’ombe ama kondoo wa hali ya juu kwenye madhabahu ya Yehova baada tu ya muda huo kuisha. Iwapo makosa mengine yangetendwa, iliwabidi wafunge kwa siku tatu mbele za Yehova, wakiomba neema Yake. Hawakumwabudu Yehova kwa sababu tu sheria Zake zilikuwa kali sana na za shuruti sana; walifanya hivyo kwa sababu ya neema Yake na uaminifu wao Kwake. Kwa hivyo, hadi leo, wameendelea kuwa waaminifu vivyo hivyo katika huduma yao, na hawajawahi kulegeza maombi waliyotoa mbele za Yehova. Siku hizi, Waisraeli bado wanapokea utunzaji na ulinzi Wake, na Yeye bado ndiye neema kati yao,

inayowafuata siku zote. Wote wanajua jinsi wanavyopaswa kumcha Yehova, na jinsi wanavyopaswa kumhudumia, na wote wanajua jinsi wanavyopaswa kutenda ili wapokee utunzaji na ulinzi Wake; hii ni kwa sababu wote wanamcha mioyoni mwao. Siri ya mafanikio ya huduma yao yote ni uchaji tu. Kwa hivyo, nyote mko vipi siku hizi? Je, mna mfanano wowote na Waisraeli? Je, unafikiri kwamba kuhudumu siku hizi ni sawa na kufuata uongozi wa mtu mkuu wa kiroho? Hamna uaminifu ama uchaji wowote kabisa. Mnapokea neema nyingi, na mnalingana na makuhani wa Israeli kwa kuwa ninyi nyote mnamhudumia Mungu moja kwa moja. Ingawa hamwingii hekaluni, yale mnayopata na yale mnayoyaona ni mengi zaidi kuliko yale ambayo makuhani waliomhudumia Yehova hekaluni walipokea. Hata hivyo, mnaasi na kupinga mara nyingi zaidi kuliko walivyofanya. Uchaji wenu ni mdogo sana, na kwa hivyo, mnapokea neema kidogo sana. Ingawa mnatoa kidogo sana, mmepokea mengi zaidi kuliko yale ambayo Waisraeli hao waliwahi kupokea. Je, katika haya yote, hamjatendewa kwa ukarimu? Wakati ambapo kazi huko Israeli ilikuwa ikifanyika, watu hawakuthubutu kumhukumu Yehova jinsi walivyotaka. Na kuwahusu ninyi, je? Insingekuwa kwa ajili ya kazi ambayo Ninaifanya sasa ili kuwashinda, Ningewezaje kuvumilia ninyi kuliaibisha jina Langu kwa ukatili sana hivi? Iwapo enzi mnayoishi ingekuwa Enzi ya Sheria, basi kwa kuzingatia maneno na matendo yenu, hakuna hata mmoja wenu angeendelea kuishi. Uchaji wenu ni mdogo sana! Daima mnanilaumu kwa kutowapa fadhila nyingi, na hata mnadai kwamba Siwapi maneno ya kutosha ya baraka, na kwamba Ninawalaani tu. Je, hamjui kwamba kwa kunicha kwa kiasi kidogo hivyo haiwezekani kwenu kukubali baraka Zangu? Je, hamjui kwamba Ninawalaani na kuwahukumu daima kwa sababu ya huduma yenu duni? Je, ninyi nyote mnahisi kwamba mmekosewa? Je, Ninawezaje kulipa baraka Zangu kundi la watu ambao ni waasi na wasiotii? Je, Nawezaje kuwapa neema Yangu kiholela watu wanaolifedhehesha jina Langu? Tayari mmetendewa kwa wema mwingi sana. Waisraeli wangelikuwa waasi kama mlivyo leo, Ningeliwaangamiza kitambo. Hata hivyo, Ninawatendea kwa huruma tu. Je, huu si ukarimu? Je, mnataka baraka nyingi zaidi kuliko hizi? Yehova huwabariki tu wale wanaomcha. Yeye huwaadibu watu wanaomwasi, Asimsamehe hata mmoja wao. Je, ninyi watu wa leo, msiojua jinsi ya kuhudumu, hamhitaji kuadibiwa na kuhukumiwa zaidi, ili mioyo yenu iweze kugeuzwa kabisa? Je, kuadibu na hukumu za aina hii si baraka bora kabisa kuwapa? Je, hizo si ulinzi wenu bora kabisa? Bila hizo, kuna yeyote kati yenu ambaye angeweza kuvumilia moto uchomao wa Yehova? Iwapo kweli mngeweza kuhudumu kwa uaminifu kama Waisraeli, je, pia hamngekuwa na neema kama mwandani wenu wa daima? Je, hamngekuwa na furaha na fadhila ya kutosha kila mara? Je, ninyi nyote mnajua jinsi mnavyopaswa kuhudumu?

Matakwa mnayohitaji kutimiza leo—kufanya kazi pamoja kwa upatanifu—ni sawa na huduma ambayo Yehova alitaka kutoka kwa Waisraeli: Vinginevyo, acheni tu kufanya huduma.

Kwa sababu ninyi ni watu wanaomhudumia Mungu moja kwa moja, angalau lazima muweze kuwa waaminifu na watiifu katika huduma yenu, na pia lazima muweze kupata mafunzo kwa njia ya utendaji. Kwa wale kati yenu wanaofanya kazi kanisani hasa, je, kuna yeyote kati ya akina ndugu walio chini yenu anayeweza kuthubutu kuwashughulikia? Je, mtu yeyote anaweza kuthubutu kuwaambia makosa yenu ana kwa ana? Mko juu ya wengine wote, mnatawala kama wafalme! Hata hamchunguzi ama kuingia katika mafunzo ya utendaji ya aina hii, lakini bado mnazungumza kuhusu kumhudumia Mungu! Kwa sasa, unaombwa uyaongoze makanisa kadhaa, lakini hukosi tu kujitolea, bali hata unashikilia mawazo na maoni yako mwenyewe, ukisema mambo kama, “Nadhani suala hili linapaswa kutendwa kwa namna hii, kwa kuwa Mungu amesema kwamba hatupaswi kuzuiliwa na wengine na kwamba siku hizi hatupaswi kutii bila kufikiria.” Kwa hivyo, kila mmoja wenu anashikilia maoni yake mwenyewe, na hakuna anayemtii mwenzake. Ingawa unajua vyema kwamba huduma yako ina shida kubwa, bado unasema, “Jinsi nionavyo, njia yangu ni sahihi kiasi. Haidhuru, kila mmoja wetu ana upande wake: Wewe zungumzia upande wako, nami nitazungumzia upande wangu; wewe shiriki kuhusu maono yako, nami nitazungumzia kuingia kwangu.” Kamwe huwajibikii mambo mengi ambayo yanapaswa kushughulikiwa, ama unaridhika tu, kila mmoja wenu akijadili maoni yake mwenyewe na kuilinda hadhi, sifa na heshima yake mwenyewe kwa uangalifu. Hakuna yeyote kati yenu aliye tayari kujinyenyekeza, na hakuna atakayechukua hatua ya kwanza kujitolea na kufidiana kasoro zenu ili maisha yasonge mbele upesi zaidi. Mnaposhirikiana pamoja, mnapaswa kujifunza kuutafuta ukweli. Unaweza kusema, “Sielewi vyema kuhusu kipengele hiki cha ukweli. Je, una uzoefu upi kuuhusu?” Ama unaweza kusema, “Una uzoefu mwingi kuniliko kuhusu kipengele hiki; tafadhali unaweza kuniongoza kiasi?” Je, hiyo haitakuwa njia nzuri ya kulitatua? Mmesikiliza mahubiri mengi, na mna uzoefu kiasi kuhusu kufanya huduma. Msipojifunza kutoka kwa kila mmoja, msaidiane, na kufidiana dosari zenu mnapofanya kazi makanisani, basi mnawezaje kupata mafunzo yoyote? Wakati wowote mnapokabiliwa na chochote, mnapaswa kufanya ushirika ninyi kwa ninyi ili maisha yenu yaweze kufaidika. Aidha, mnapaswa kufanya ushirika kwa makini kuhusu mambo ya aina yoyote kabla kufanya maamuzi yoyote. Ni kwa kufanya hivyo tu ndipo mnawajibikia kanisa badala ya kutenda kwa uzembe tu. Baada ya kutembelea makanisa yote, mnapaswa kukusanyika pamoja na kushiriki kuhusu masuala yote mnayogundua na matatizo yoyote mliyokumbana nayo katika kazi yenu, na kisha mnapaswa kuwasiliana kuhusu nuru na mwangaza ambao mmepokea—huu ni utendaji wa msingi wa huduma. Lazima mfanikishe ushirikiano wa upatanifu kwa ajili ya kazi ya Mungu, kwa manufaa ya kanisa, na ili muwahimize ndugu zenu mbele. Mnapaswa kushirikiana, kila mmoja akimrekebisha mwenzake na kufikia matokeo bora ya kazi, ili kuyatunza mapenzi ya Mungu. Hii ndiyo maana ya ushirikiano wa kweli, na ni wale tu wanaoshiriki katika ushirikiano huo ndio watakaopata kuingia kwa kweli. Mnaposhirikiana, baadhi ya maneno mnayozungumza

yanaweza kuwa yasiyofaa, lakini hilo si muhimu. Shirikini kulihusu baadaye, na mlielewe vyema; msilipuuze. Baada ya ushirika wa aina hii, mnaweza kufidia kasoro za ndugu zenu. Ni kwa kusonga kwa kina daima katika kazi yenu kwa namna hii ndipo mnaweza kupata matokeo bora. Kama watu wanaomhudumia Mungu, kila mmoja wenu lazima aweze kulinda maslahi ya kanisa katika kila kitu mnachofanya, badala ya kuzingatia tu masilahi yenu wenyewe. Haikubaliki ninyi kutenda kila mtu peke yake, daima mkidhoofishana. Watu wanaotenda kwa namna hiyo hawafai kumhudumia Mungu! Watu kama hao wana tabia mbaya sana; hawana ubinadamu hata kidogo ndani yao. Wao ni Shetani asilimia mia moja! Wao ni wanyama! Hata sasa, mambo kama haya bado hutokea miongoni mwenu; hata mnafika kiasi cha kushambuliana wakati wa ushirika; mkitafuta visingizio kwa makusudi na kughadhabika sana mnapogombana kuhusu suala fulani lisilo la maana, pasiwe na mtu aliye radhi kujiweka kando, kila mtu akimfichia mwenzake fikira zake za ndani, akimtazama yule mwingine kwa makini na kuwa mwangalifu daima. Je, tabia ya aina hii inafaa katika kumhudumia Mungu? Je, kazi kama hiyo yako inaweza kuwapa ndugu zako chochote? Huwezi tu kuwaongoza watu kwenye njia sahihi ya maisha, lakini kwa kweli unawajaza ndugu zako tabia zako potovu. Je, huwadhuru wengine? Dhamiri yako ni mbaya na ni mbovu kabisa! Huingii katika uhalisi, wala huuweki ukweli katika vitendo. Aidha, unawafichulia wengine asili yako mbaya mno bila aibu. Huna aibu hata kidogo! Umeaminiwa ndugu hawa, lakini unawapeleka kuzimuni. Je, wewe si mtu ambaye dhamiri yake imekuwa mbovu? Huna aibu hata kidogo!

Kuboresha Ubora wa Tabia ni Kwa Ajili ya Kupokea Wokovu wa Mungu

Kuendeleza ubora wa tabia ya watu kunahitaji kwamba muendeleze uwezo wenu wa kupokea, Ili muweze kuelewa maneno ya Mungu na kujua jinsi ya kutenda kulingana nayo. Hili ndilo hitaji la msingi kabisa. Je, siyo imani iliyovurugika ikiwa unanifuata bila kufahamu kile Ninachosema? Haidhuru ni maneno mangapi Ninayosema, ikiwa hamuwezi kufika hapo, ikiwa hamuwezi kuyaelewa bila kujali Ninachosema, hii inamaanisha mna upungufu wa ubora wa tabia. Ni kwa sababu hamiliki uwezo wa kupokea kwamba hamna ufahamu hata mdogo wa kile Ninachosema. Kwa hivyo, ni vigumu sana kutimiza matokeo yanayotamanika. Mambo mengi hayawezi kusemwa kwenu moja kwa moja na athari ya awali haiwezi kutimizwa. Kwa hiyo, kazi za ziada zinapaswa kuongezwa kwa kazi Yangu. Ni muhimu kuzindua kazi hii ya “kuinua ubora wa tabia ya watu” miongoni mwenu kwa sababu uwezo wenu wa kupokea, uwezo wa kuona mambo, na viwango ambavyo kwavyo mnaishi vimepungukiwa sana, kazi ya “uinuaji wa ubora wa tabia” sharti ifanywe ndani yenu. Hili ni jambo lisiloepukika, na hakuna mbadala. Ni kwa njia hii tu ndiyo matokeo fulani yanaweza kutimizwa; la sivyo, maneno yote

Ninayosema hayatafanikiwa, na hamngekumbukwa kama wenye dhambi? Je! Hamngekuwa wapotovu? Je, hamjui ni kazi gani inayofanywa kwenu na ni nini kinachohitajika kutoka kwenu? Mnapaswa kujua ubora wenu wenyewe wa tabia; hauwezi kufikia kile Ninachohitaji kamwe. Je, hii haicheleweshi kazi? Kwa ubora wa tabia na hulka yenu ya sasa, hakuna hata mmoja wenu ambaye anafaa kushuhudia kwa ajili Yangu, na hakuna mtu anayewezana na kazi ya kulichukua jukumu kubwa la kazi Yangu ya baadaye. Je, hamhisi aibu sana? Mkiendelea kwa njia hii, mnawezaje kuyaridhisha mapenzi Yangu? Unapaswa kuishi maisha yako kikamilifu. Usiruhusu muda upite bure. Hakuna thamani katika kufanya hivyo. Unapaswa kujua mambo ambayo inabidi kujiandaa nayo. Usijione kuwa mjuaji wa kila kitu. Hukaribii hata kidogo! Je! Kuna nini cha kuzungumzia ikiwa huna hata ufahamu wa kimsingi wa ubinadamu? Je, si vyote havingekuwa na maana? Na kwa hivyo hakuna hata mmoja wenu aliye na ubinadamu na ubora wa tabia ninaohitaji kwa ukamilifu. Ni vigumu kupata mtu ambaye anafaa kutumiwa. Mnaamini ninyi ni watu ambao wanaweza kufanya kazi kubwa zaidi kwa ajili Yangu na kujitwika ukabidhi mkubwa kutoka Kwangu. Kwa kweli, hamjui jinsi hata ya kuingia katika masomo mengi mbele yenu, hivyo ingewezekanaje kuingia katika kweli za kina? Kuingia kwenu kunapaswa kufuata mpangilio na kwa viwango. Hakupaswi kuwa kwa vurugu—hiyo haina manufaa. Anzeni na uingiaji wa juu juu kabisa: Yasome maneno haya mstari kwa mstari hadi mfikie ufahamu na ubayana. Mnaposoma maneno ya Mungu, msiyapitie kwa juu juu tu kana kwamba unapendezwa na maua huku ukienda shoti mgongoni mwa farasi, na usilifanye kwa namna isiyo ya dhati. Unaweza pia kusoma baadhi ya vitabu vya kumbukumbu mara kwa mara (kama vile vitabu juu ya sarufi au vya balagha) ili kukuza maarifa yako. Usisome vitabu kama vile riwaya za mapenzi, wasifu za watu mashuhuri au vile vinavyohusu sayansi ya kijamii; hivi havina manufaa, na vinaweza tu kusababisha. Lazima uwe mweledi wa yote unayopaswa kuingia na unapaswa kufahamu. Madhumuni ya kuendeleza ubora wa tabia sio mengine ila kuwasaidia watu kujua asili yao wenyewe, utambulisho, hadhi na thamani. Unapaswa kuelewa kwa nini lazima watu wafuatilie ukweli katika kumwamini Mungu, na iwapo inakubalika kwa watu kutoinua ubora wao wa tabia. Ni muhimu kwamba ujielimishe kila wakati; ni sharti usitupe hili mbali! Lazima uelewe kwa nini ubora wa tabia wa watu sharti uinuliwe, jinsi unavyopaswa kuinuliwa, na ni vipengele vipi unavyopaswa kuingia katika. Lazima muelewe maana ya kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida, kwa nini kazi hii inapaswa kufanywa, na jinsi watu wanapaswa kuratibu. Katika kuelimika, mnapaswa kuwa dhahiri kuhusu vipengele vipi vinayopaswa kufunzwa, na jinsi gani mtu anapaswa kuingia. Nyote mnapaswa kujua lengo la kuelimika ni nini. Je, sio kuyafahamu maneno ya Mungu na kuingia katika ukweli? Hali inayosambaa makanisani sasa ni ipi? Mkimwomba mtu apate kuelimika, anasahau kuhusu furaha ya maneno ya Mungu. Hafanyi chochote siku nzima kando na kuelimishwa. Mkimhitaji kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida, anashughulikia tu kuisafisha nyumba yake, kupika, au

kununua vyombo vya kupika. Anajali tu kuhusu mambo haya na hajui jinsi ya kuishi maisha ya kanisa kwa kawaida. Umepotoka katika matendo yako ikiwa unabaki katika hali ya sasa. Basi kwa nini unaombwa kuingia katika maisha ya kiroho? Yote unayojifunza ni mambo haya ambayo hayawezi kukusaidia kufikia kile kinachohitajika kwako. Jambo la muhimu zaidi bado ni kuingia kwa maisha. Sababu ya kufanya kazi hii ni kutatua shida ambazo watu hukumbana nazo katika uzoefu wao. Kuinua ubora wa tabia kunakuruhusu kujua ubinadamu na kiini cha mwanadamu—kusudi kuu la kuyajua mambo haya ni ili maisha ya watu ya kiroho yaweze kukua na tabia yao iweze kubadilika. Unaweza kujua jinsi ya kuvaa na kupendeza; unaweza kuwa na utambuzi na hekima, na hata hivyo hatimaye, siku inapokuja kwako kuenda kazini, unashindwa kufanya hivyo. Unapaswa kujua, kwa hiyo, kile unapaswa kufanya pia wakati unainua ubora wako wa tabia. Kukubadilisha ni lengo. Kuinua ubora wa tabia ni jambo la ziada. Haitakubalika kama ubora wako wa tabia hauendelezwi. Ni vibaya hata zaidi ikiwa tabia yako haiwezi kubadilishwa. Moja bila ya nyingine haitoshi. Kuwa na ubinadamu wa kawaida hakumaanishi kwamba umekuwa na ushuhuda mkubwa sana. Kile kinachohitajika kwako si rahisi sana.

Wakati ambapo ubora wa tabia ya mtu umeendelea kiasi kwamba ana hisia na mtindo wa maisha ya ubinadamu wa kawaida na pia kuwa na kuingia kwa maisha, ni hapo tu ndipo ataweza kubadilika na kushuhudia. Siku ya kutoa ushuhuda inapofika, pia kuna haja ya kuzungumza kuhusu mabadiliko katika maisha ya binadamu na kuhusu ufahamu wa Mungu ndani. Mchanganyiko wa vipengele hivi viwili tu ndio ushahidi wa kweli na faida yako ya kweli. Haitakubalika ikiwa una mabadiliko tu katika ubinadamu kwa nje na huna ufahamu kwa ndani. Haitakubalika pia ikiwa una ufahamu na ukweli kwa ndani lakini hutili maanani kuishi kulingana na ubinadamu wa kawaida. Kazi inayofanyika kwako leo sio kuwaonyesha wengine bali kukubadilisha. Unahitaji tu kuzingatia kujibadilisha. Unaweza kuandika na kusikiliza kila siku, lakini haitawezekana ikiwa hushiriki katika maeneo mengine ya maisha yako. Unapaswa kuwa na kuingia katika kila kipengele. Unapaswa kuwa na maisha ya kawaida ya mtakatifu. Akina dada wengi huvaa kama wanawake matajiri na kaka wanavaa kama waungwana matajiri au mabwana, wakupoteza kabisa ustahifu wa watakatifu. Kipengele kimoja ni kuinua ubora wa tabia ya mtu, ambacho kinaweza kufanikishwa kwa kawaida. Kipengele kingine cha umuhimu mkubwa ni kula na kunywa maneno ya Mungu. Je, haingekuwa kupoteza elimu ikiwa ubora wako wa tabia umeinuliwa lakini haukukutumiwa kwa sababu hukula na kunywa maneno ya Mungu? Lazima vipengele vyote viwili viunganishwe. Kwa nini maarifa ya Mungu yanatajwa katika majadiliano ya kile kinachohitajika kwako? Je, hii si kwa ajili ya matokeo ya kazi ya baadaye? Baada yako kushindwa, lazima uweze kushuhudia kutokana na uzoefu wako mwenyewe. Haitakubalika kama sura yako ya nje ni moja ya ubinadamu wa kawaida lakini huwezi kuonyesha uzoefu wako kupitia kinywa chako. Unapokuwa na maisha ya kawaida ya

kiroho, unapaswa kufikia ubinadamu wa kawaida, na vipengele vingi vya ubinadamu wa kawaida vitaweza kufunzwa kwa dhahiri. Je, ungesema kwamba kufagia sakafu kunahitaji mafunzo maalum? Ikiwa unahitaji kutumia saa moja kufanya mazoezi jinsi ya kushikilia vijiti kwa kula, hiyo haikubaliki hata zaidi! Ni nini kinashirikishwa ndani ya ubinadamu wa kawaida? Utambuzi, hisia, dhamiri na tabia. Iwapo unaweza kufanikisha ukawaida katika kila mojawapo ya vipengele hivi, ubinadamu wako uko katika kiwango kinachostahili. Unapaswa kuwa na mfanano wa binadamu wa kawaida na utende kama anayemwamini Mungu. Sio lazima ufikie viwango vya juu zaidi au kujishughulisha na diplomasia. Unapaswa tu kuwa mwanadamu wa kawaida, na hisia za kawaida za mtu, uweze kung'amua vitu, na kwa kiwango cha chini uonekane kama mwanadamu wa kawaida. Hiyo itakuwa imetoshwa. Kila kitu kinachohitajika kwako leo kiko katika uwezo wako, na huku si kukulazimisha ufanye kadri ya uwezo wako hata kidogo. Hakuna maneno yasiyo na maana au kazi isiyofaa yatakayotekelezwa kwako. Uovu wote ulioonyeshwa au kufichuliwa katika maisha yako lazima uondolewe. Ninyi mmepotoshwa na Shetani na mna sumu nyingi sana za Shetani. Yote ambayo yanahitajika kwako ni kuiepuka tabia hii potovu ya kishetani, si wewe kuwa mtu mwenye cheo cha juu, au mtu maarufu au mkuu. Hii haina maana. Kazi ambayo imefanyika kwenu inaafikiana na kile ambacho ni cha asili kwenu. Kuna mipaka ya kile Ninachohitaji kutoka kwa watu. Ikiwa watu wa leo wote wangeombwa kutenda kama maafisa wa serikali, na kujizoeza toni ya sauti ya maafisa wa serikali, kujifunza katika namna ya kuzungumza ya viongozi wa serikali wenye cheo cha juu, au kujifunza kwa namna na sauti ya kuzungumza ya waandishi wa insha na waandishi wa riwaya, basi hili halingekubalika pia. Halingeweza kufikiwa. Kwa mujibu wa ubora wa tabia zenu, mnapaswa angalau kuweza kuzungumza kwa hekima na busara na kuelezea mambo wazi. Ni wakati huo ndipo mtakapoyatosheleza mahitaji. Kwa kiwango kidogo sana, utambuzi na hisia vinapaswa kufikiwa. Kwa sasa jambo kuu ni kuitupilia mbali tabia potovu ya kishetani. Lazima uutupilie mbali uovu unaouonyesha. Ikiwa hujavitupilia mbali hivi, unawezaje kugusia hisia na utambuzi wenye mamlaka mkubwa kabisa? Watu wengi wanaona kwamba enzi imebadilika. Hivyo hawajizoezi unyenyekevu au uvumilivu wowote, na pengine pia hawana upendo wowote au mwenendo mwema wa kitakatifu pia. Watu hawa ni wajinga mno! Je, wana kiwango chochote cha ubinadamu wa kawaida? Je, wanao ushuhuda wowote wa kuzungumziwa? Hawana utambuzi na hisia zozote kamwe. Bila shaka, vipengele fulani vya utendaji wa watu vilivyopotoka na vyenye makosa vinapaswa kurekebishwa. Kama vile maisha ya watu ya kiroho yasiyopindika ya zamani au mwonekano wao wenye ganzi na upumbavu—vitu hivi vyote vinapaswa kubadilika. Mabadiliko hayamaanishi kukuruhusu uwe mpotovu au kujiingiza katika mwili, kusema chochote utakacho. Kuzungumza kiholela hakuwezi kukubalika. Kutenda kama mwanadamu wa kawaida ni kuzungumza kwa kueleweka. Ndiyo inamaanisha ndiyo, na la inamaanisha la. Kuwa mwenye ukweli kwa uhakika na uzungumze inavyofaa. Usilaghai, usidanganye. Inapaswa

kujulikana ni mipaka gani mtu wa kawaida anaweza kufikia kuhusu mabadiliko ya tabia. Ikiwa hiyo haijulikani, hutaweza kuingia katika uhalisi.

Umuhimu wa Kuukoa Uzao wa Moabu

Katika miaka hii miwili hadi mitatu ya kazi, kile kilichopaswa kutimizwa katika kazi ya hukumu iliyofanyika juu yenu kimetimizwa kimsingi. Watu wengi wameacha matarajio na kudura yao ya baadaye kiasi. Hata hivyo, inapotajwa kuwa ninyi ni uzao wa Moabu, wengi kati wenu huchukizwa sana—nyuso zenu hubadilika, vinywa vyenu hupinda, na macho yenu hukodolea. Hamuwezi kabisa kuamini kwamba ninyi ni uzao wa Moabu. Moabu ilifukuzwa hadi nchi hii baada ya kulaaniwa. Ukoo wa wana wa Moabu umerithishwa mpaka leo, na ninyi nyote ni uzao wake. Hakuna kitu ambacho Ninaweza kufanya—nani aliyekusababisha uzaliwe katika nyumba ya Moabu? Ninakuhurumia na Siko radhi uwe hivi, lakini ukweli hauwezi kubadilishwa na watu. Wewe ni uzao wa Moabu, na Siwezi kusema kuwa wewe ni uzao wa Daudi. Haijalishi wewe ni uzao wa nani, bado wewe ni mmoja wa viumbe. Ni kwamba tu wewe ni kiumbe wa cheo cha chini—wewe ni kiumbe wa kuzaliwa katika hali duni. Viumbe vyote lazima vipitie kazi yote ya Mungu, vyote ni vyombo vya kushinda Kwake, na lazima vyote viione tabia Yake yenye haki, na kupitia hekima na kudura Yake. Sasa wewe ni uzao wa Moabu na lazima uikubali hukumu hii na kuadibu, hivyo kama hungekuwa uzao wa Moabu, basi pia hungehitaji kukubali hukumu na kuadibu huku? Unapaswa kutambua hili! Kwa kweli, kufanya kazi kwa uzao wa Moabu kwa sasa ni kwa thamani sana na kwenye umuhimu sana. Maadam kazi imefanywa kwenu, ina umuhimu mkubwa mno. Kama kazi ingefanywa kwa uzao wa Hamu haingeweza kuwa muhimu kwa sababu wao hawajazaliwa katika hali duni kama hiyo na kuzaliwa kwao sio sawa na Moabu. Uzao wa mwana wa pili wa Nuhu Hamu umelaaniwa tu—hawakuja kutokana na uasherati. Ni kwamba tu wao ni wa hali ya chini, kwa sababu Nuhu aliwalaani na wao ni watumishi wa watumishi. Wanayo hali ya chini, lakini thamani yao ya asili haikuwa chini. Tukizungumza kuhusu Moabu, watu wanajua kwamba awali alikuwa na hali ya chini kwa sababu alizaliwa kutokana na uasherati. Ingawa nafasi ya Loti ilikuwa ya juu sana, Moabu alizaliwa na Lutu na binti yake. Lutu aliitwa mtu mwenye haki, lakini Moabu bado alikuwa amelaaniwa. Moabu alikuwa wa thamani ya chini na alikuwa na cheo cha chini, na hata kama hakuwa amelaaniwa alikuwa wa uchafu, hivyo alikuwa tofauti na Hamu. Hakukubali na alipinga, aliasi dhidi ya Yehova, ndiyo sababu alianguka katika maeneo yenye giza zaidi. Kufanya kazi sasa kwa uzao wa Moabu ni kuwaokoa wale ambao wameanguka katika giza zaidi. Ingawa walikuwa wamelaaniwa, Mungu yuko tayari kupata utukufu kutoka kwao. Hii ni kwa sababu hapo awali, wote walikuwa watu waliomkosa Mungu mioyoni mwao—kuwafanya tu kuwa wale wanaomtii na kumpenda Yeye ni ushindi wa kweli, na matunda hayo ya kazi ni ya thamani sana na yenye kuridhisha zaidi. Huku tu ni kupata utukufu—huu ndio utukufu ambao Mungu anataka

kuupata katika siku za mwisho. Ingawa watu hawa ni wa nafasi ya chini, sasa wanaweza kupata wokovu mkubwa mno, ambao kwa kweli ni kupandishwa hadhi na Mungu. Kazi hii ni ya maana sana, na ni kwa njia ya hukumu ndipo Anawapata watu hawa. Yeye hawaadhibu kwa makusudi, lakini Amekuja kuwaokoa. Kama angekuwa Anafanya kazi ya kushinda katika Israeli wakati wa siku za mwisho ingekuwa ni bure; hata kama ingezaa matunda, haingekuwa na thamani yoyote au umuhimu wowote mkubwa, na Yeye hangeweza kupata utukufu wote. Anafanya kazi kwenu, yaani, wale ambao wameanguka katika maeneo yenye giza zaidi, wao walio nyuma zaidi kimaendeleo. Watu hawa hawakiri kuwa kuna Mungu na kamwe hawajapata kujua kwamba kuna Mungu. Viumbe hawa wamepotoshwa na Shetani hadi kiwango ambapo wamemsahau Mungu. Wamepofushwa na Shetani na hawajui kabisa kwamba kuna Mungu mbinguni. Katika mioyo yenu nyote mnaabudu sanamu, mnamwabudu Shetani—je, si ninyi ni watu wa hali ya chini zaidi, watu walio nyuma zaidi kimaendeleo? Ninyi ni wa hali ya chini kabisa ya mwili, mnakosa uhuru wowote wa kibinafsi, na mnapitia shida pia. Ninyi pia ni watu mlio katika ngazi ya chini kabisa katika jamii hii, bila hata uhuru wa imani. Huu ni umuhimu wa kufanya kazi kwenu. Kufanya kazi kwenu sasa, uzao wa Moabu, sio kuwafedhehesha kwa makusudi, lakini ni kufichua umuhimu wa kazi. Ni kuwainua sana. Ikiwa mtu ana mantiki na utambuzi, atasema: “Mimi ni uzao wa Moabu. Kweli sistahili kuinuliwa kukuu huku na Mungu ambako nimepokea sasa, au baraka hizi nyingi. Kwa mujibu wa yale ninayofanya na kusema, na kulingana na hali na thamani yangu—sistahili kabisa hizo baraka nyingi kutoka kwa Mungu. Waisraeli wana upendo mkubwa kwa Mungu, na neema wanayoifurahia imefadhiliwa kwao na Yeye, lakini hali yao ni ya juu zaidi kuliko yetu. Abrahamu alijitolea sana kwa Yehova, na Petro alijitolea sana kwa Yesu—ibada yao ilishinda yetu kwa mara mia, na kwa msingi wa matendo yetu hatufai kabisa kufurahia neema ya Mungu.” Huduma ya watu hawa nchini China haiwezi kuletwa mbele za Mungu hata kidogo. Ni fujo kamili tu, na kwamba sasa mnafurahia neema nyingi za Mungu ni kuinuliwa na Mungu kabisa! Je, ni wakati upi mmeitafuta kazi ya Mungu? Je, mmeyatoa maisha yenu kwa Mungu lini? Ni wakati gani mmeiacha familia yako kwa urahisi, wazazi wenu, na watoto wenu? Hakuna hata mmoja wenu aliyelipa gharama kubwa! Kama haingekuwa kwa Roho Mtakatifu kukufanya uonekane, wangapi wenu wangeweza kutoa dhabihu kila kitu? Ni kwa sababu tu mmelazimishwa na kushurutishwa ndipo mmefuata hadi leo. Ibada yenu iko wapi? Utiifu wenu uko wapi? Kulingana na matendo vyenu, mngepaswa kuangamizwa muda mrefu uliopita—mngeondolewa kabisa. Nini kinawafanya mstahili kufurahia baraka nyingi mno? Hamstahili hata kidogo! Nani kati yenu amebuni njia yake mwenyewe? Ni nani kati yenu ameipata njia ya ukweli mwenyewe? Ninyi nyote ni wavivu na walafi, fidhuli msio na maana ambao mnasherehekea katika faraja kwa tamaa! Mnafikiri ninyi ni wakubwa sana? Je, nini mlikho nacho cha kujivunia? Hata kama Singesema ninyi ni uzao wa Moabu, je, asili yenu, mahali penu pa kuzaliwa ni ya fahari sana? Hata kama Singesema ninyi ni uzao wake, je, si ninyi

nyote ni uzao wa Moabu kwa kweli? Ukweli wa mambo unaweza kubadilishwa? Je, kufichua asili yenu sasa kunaenda dhidi ya ukweli wa mambo? Angalieni jinsi mlivyo wanyonge, maisha yenu, na tabia—je, hamjui kwamba ninyi ni wa chini kabisa kati ya walio chini miongoni mwa wanadamu? Nini mlichio nacho cha kujisifia? Angalia nafasi yenu katika jamii. Je, si mko katika kiwango cha chini kabisa? Je, mnadhani kwamba Nimenena vibaya? Ibrahimu alimtoa Isaka. Nini ambacho mmetoa? Ayubu ilitoa kila kitu. Nini ambacho mmetoa? Watu wengi sana wameyatao maisha yao, wakafa, wakamwaga damu yao ili kutafuta njia ya kweli. Je, mmelipa gharama hiyo? Kwa kulinganisha, hamna sifa zinazostahili hata kidogo kufurahia neema hiyo kubwa, kwa hivyo ni sawa kusema leo kwamba ninyi ni uzao wa Moabu? Msijione kuwa wakuu sana. Huna chochote cha kujisifia. Wokovu mkubwa kama huo, neema hiyo kubwa imepewa kwenu bure. Hamjatoa chochote, lakini mmeifurahia neema bure. Je, hamuoni haya? Je, njia hii ya ukweli ni jambo ambalo ninyi wenyewe mlipata kupitia kutafuta? Je, si ni Roho Mtakatifu aliyewalazimisha kuikubali? Kamwe hamkuwa na moyo wa kutafuta na hasa hamkuwa na mioyo ya kuutafuta ukweli, ya kuutamani ukweli. Mmekuwa tu mkistarehe na kuufurahia, na mmeupata ukweli huu bila jitihada kwa upande wenu. Mna haki gani ya kulalamika? Je, unadhani kuwa wewe ni wa thamani kubwa zaidi? Ikilinganishwa na wale ambao walitoa dhambi maisha yao na kumwaga damu yao, nini mnachopaswa kulalamikia? Kuwaangamiza hivi sasa litakuwa ni jambo linalotarajiwa! Kando na kutii na kufuata, hamna chaguzi zingine. Ninyi hamstahili kabisa! Wengi wa wale kati yenu waliitwa, lakini kama mazingira hayangewalazimisha au kama hamngeitwa, hamngekuwa tayari kabisa kutokea wazi. Nani yuko tayari kutelekeza mambo kwa namna hii? Ni nani yuko tayari kuacha anasa za mwili? Ninyi nyote ni watu ambao husherehekea kwa ulafi katika faraja na kutafuta maisha ya anasa! Mmepata baraka nyingi mno—nini kingine mnacho cha kusema? Mna malalamiko yapi? Mmefurahia baraka nyingi mno na neema kuu mno mbinguni, na kazi sasa imefichuliwa kwenu ambayo haikuwahi kufanywa duniani awali. Je, si hii ni baraka? Kwa sababu mmempinga na kuasi dhidi ya Mungu, sasa mmepitia kuadibu kiasi hiki. Kwa sababu ya kuadibu huku mmeziona rehema na upendo wa Mungu, na hata zaidi mmeziona haki na utakatifu Wake. Kwa sababu ya kuadibu huku na kwa sababu ya uchafu wa wanadamu, mmeiona nguvu kuu ya Mungu, na mmeuona utakatifu na ukuu Wake. Je, si huu ni ukweli adimu mno? Je! Si haya ni maisha yenye maana? Kazi ambayo Mungu hufanya ina maana tele! Hivyo nafasi yenu ilivyo chini zaidi, ndivyo inavyoonyesha zaidi kuinuliwa na Mungu, na ndivyo inavyothibitisha zaidi jinsi kazi Yake ilivyo na thamani kwenu leo. Ni hazina yenye thamani mno hasa! Haiwezi kupatikana popote pengine! Kwa muda mrefu hakuna mtu aliyefurahia wokovu mkubwa hivi. Ukweli kwamba nafasi yenu ni ya chini inaonyesha jinsi wokovu wa Mungu ulivyo mkuu, na inaonyesha kwamba Mungu ni mwaminifu kwa wanadamu—Yeye huokoa, sio kuangamiza.

Watu wa Uchina hawajawahi kumwamini Mungu na hawajawahi kumhudumia Yehova, hawajawahi kumhudumia Yesu. Yote wanayofanya ni kusujudu, kufukiza uvumba, kuchoma sanamu ya Mungu ya karatasi, na kumwabudu Buddha. Wao wanaabudu sanamu tu—wote ni waasi mno, hivyo jinsi nafasi ya watu ilivyo ya chini zaidi, ndivyo inavyoonyesha zaidi kwamba kile Mungu hupata kutoka kwenu ni utukufu hata zaidi. Kutoka kwa mtazamo wa watu fulani, wangesema: “Mungu, ni kazi gani Unayofanya? Wewe, Mungu mwenye fahari sana, Mungu mtakatifu mno, ulikuja katika nchi yenye uchafu? Je, Unajidharau sana hivyo? Sisi ni wachafu sana, lakini Uko radhi kuwa pamoja nasi? Uko tayari kuishi kati yetu? Sisi ni wa cheo cha chini sana, lakini Uko radhi kutufanya kuwa kamili? Na Ungetutumia sisi kama mifano na vielelezo?” Ninasema: Huelewi mapenzi Yangu. Huelewi kazi ambayo Nataka kufanya wala huelewi tabia Yangu. Huwezi kufikia umuhimu wa kazi ambayo Ninaenda kufanya. Je, kazi Yangu ingepatana na mawazo ya kibinadamu? Kulingana na mawazo ya kibinadamu, Ningelazimika kuzaliwa katika nchi nzuri ili kuonyesha kwamba mimi ni wa hali ya juu, kuonyesha kwamba Mimi ni wa thamani kubwa, na kuonyesha kuheshimiwa Kwangu, utakatifu, na ukuu Wangu. Kama Ningezaliwa mahali ambapo pananitambua, katika familia ya ngazi ya juu, na kama Ningekuwa wa cheo na hadhi ya juu, basi Ningetendewa vizuri sana. Hiyo haingekuwa na manufaa kwa kazi Yangu, hivyo je, wokovu mkuu mno bado ungeweza kufichuliwa? Wote wanaoniona Mimi wangenitii, na hawangenajisiwa na uchafu. Nilipaswa kuzaliwa katika mahali pa aina hii. Hivyo ndivyo ninyi mnaamini. Lakini litafakari: Je! Mungu alikuja duniani kwa ajili ya raha, au kwa ajili ya kazi? Kama Ningefanya kazi katika aina ya mahali hapo rahisi, mahali penye starehe, je, Ningepata utukufu Wangu kamili? Je, Ningeweza kuvishinda viumbe Vyangu vyote? Mungu alipokuja duniani Yeye hakuwa wa ulimwengu na Yeye hakuwa mwili ili apate kuufurahia ulimwengu. Mahali ambapo kufanya kazi kungefichua tabia Yake vizuri sana na pawe mahali pa maana zaidi ni mahali Alipozaliwa. Kama ni nchi takatifu au yenye uchafu, na bila kujali Anapofanya kazi, Yeye ni mtakatifu. Kila kitu duniani kiliumbwa na Yeye; Ni kwamba tu kila kitu kimepotoshwa na Shetani. Hata hivyo, vitu vyote bado ni Vyake; vyote viko mikononi Mwake. Kuja Kwake katika nchi yenye uchafu kufanya kazi ni kufichua utakatifu Wake; Yeye hufanya hivi kwa ajili ya kazi Yake, yaani, Yeye huvumilia aibu kubwa kufanya kazi kwa njia hii ili kuwaokoa watu wa nchi hii yenye uchafu. Hii ni kwa ajili ya ushuhuda na ni kwa ajili ya wanadamu wote. Kile aina hii ya kazi inawaruhusu watu kuona ni haki ya Mungu, na ina uwezo zaidi wa kuonyesha mamlaka ya juu kabisa ya Mungu. Ukuu na uadilifu Wake vinaonyeshwa kupitia wokovu wa kundi la watu wa hali ya chini ambao hakuna mtu anayewapenda. Kuzaliwa katika nchi yenye uchafu haimaanishi kabisa kuwa Yeye ni duni; inawaruhusu tu viumbe vyote kuuona utuu Wake na upendo wake wa kweli kwa wanadamu. Zaidi Anavyofanya kwa njia hii, zaidi inavyofichua upendo Wake safi zaidi kwa mwanadamu, upendo wake usio na dosari. Mungu ni mtakatifu na mwenye haki. Hata ingawa Alizaliwa katika nchi yenye uchafu, na

ingawa Anaishi na watu hao ambao wamejawa uchafu, kama vile Yesu alivyoishi na wenye dhambi katika Enzi ya Neema, si kazi Yake yote kwa ajili ya kuishi kwa wanadamu wote? Je, si yote ni ili mwanadamu aweze kuupata wokovu mkuu? Miaka elfu mbili iliyopita Aliishi na wenye dhambi kwa miaka kadhaa. Hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya ukombozi. Leo, Anaishi na kikundi cha watu wachafu, wa hali ya chini. Hii ni kwa ajili ya wokovu. Je, si kazi Yake yote ni kwa ajili yenu, wanadamu hawa? Kama haingekuwa ili kuwaokoa wanadamu, kwa nini Angeishi na kuteswa pamoja na wenye dhambi kwa miaka mingi sana baada ya kuzaliwa horini? Na kama haingekuwa ili kuwaokoa wanadamu, kwa nini Angeurudia mwili kwa mara ya pili, kuzaliwa katika nchi hii ambako mapepo hukusanyika, na kuishi na watu hawa ambao wamepotoshwa kwa kina na Shetani? Je, si Mungu ni mwaminifu? Ni aina gani ya kazi Yake ambayo haijakuwa kwa ajili ya wanadamu? Ni aina gani ambayo haijakuwa kwa ajili ya kudura yako? Mungu ni mtakatifu. Hili haliwezi kubadilika! Yeye hanajisiwi na uchafu, ingawa Amekuja katika nchi yenye uchafu; yote haya yanamaanisha tu kwamba upendo wa Mungu kwa wanadamu ni wenye kuwajali wengine sana, mateso na aibu Anayoyavumilia ni makubwa sana! Hamjui kwamba Yeye hupitia aibu kubwa sana kwa ajili yenu wote na kwa ajili ya kudura yenu? Je, hamjui hivyo? Yeye hawaokoi watu wakuu au wana wa familia tajiri na zenye uwezo, lakini Yeye huwaokoa hasa wale ambao ni wa hali za chini na wanaodharauliwa na wengine. Je, si haya yote ni utakatifu Wake? Je, si haya yote ni haki Yake? Afadhali Azaliwe katika nchi yenye uchafu na kuteseka aibu yote kwa ajili ya kuishi kwa wanadamu wote. Mungu ni halisi sana—Hafanyi kazi ya uwongo. Je, si kila hatua ya kazi Yake imefanyika kwa utendaji hivi? Ingawa watu wote wanamkashifu na kusema kuwa Anakaa mezani pamoja na wenye dhambi, ingawa watu wote wanamdhihaki na kusema kuwa Anaishi na wana wa uchafu, na watu wa hali ya chini sana, bado Anajitolea bila ubinafsi, na bado Anakataliwa kwa njia hii kati ya wanadamu. Je, si mateso Anayoyahimili ni makubwa zaidi kuliko yenu? Je, si kazi Yake ni zaidi ya gharama ambayo mmelipa? Mlizaliwa katika nchi ya uchafu lakini mmepata utakatifu wa Mungu. Mlizaliwa katika nchi ambako mapepo hukusanyika lakini mmepokea ulinzi mkubwa. Je, mna uchaguzi gani mwingine? Ni malalamiko yapi mliyo nayo? Je, si mateso ambayo Amevumilia ni makubwa zaidi kuliko mateso ambayo mmevumilia? Amekuja duniani na hajawahi kufaidi furaha za ulimwengu wa kibinadamu. Anayachukia mambo hayo. Mungu hakuja duniani kufurahia manufaa ya kibinadamu kutoka kwa mwanadamu, wala haikuwa kufurahia mambo mazuri ya wanadamu kula na kuvalia. Hazingatii mambo haya; Alikuja duniani kuteseka kwa ajili ya mwanadamu, si kufurahia mambo mazuri ya kidunia. Alikuja kuteseka, Alikuja kufanya kazi, na kukamilisha mpango Wake wa usimamizi. Hakuchagua mahali pazuri, kuishi katika ubalozi au hoteli ghali mno, wala Hana watumishi kadhaa kumtumikia. Kutokana na kile mmeona, hamjui kama Alikuja kufanya kazi au kufurahia? Je, macho yenu hayafanyi kazi? Amewapa kiasi gani? Kama Angezaliwa katika mahali pazuri Angeweza kuupata utukufu? Je, Angeweza kufanya

kazi? Je! Huko kungekuwa na umuhimu wowote? Angeweza kuwashinda kabisa wanadamu? Angeweza kuwaokoa watu kutoka katika nchi ya uchafu? Kulingana na mawazo ya kibinadamu, “Mungu, kwa kuwa Wewe ni mtakatifu, kwa nini Ulizaliwa katika mahali penye uchafu mno kama hapa? Unatuchukia na kutukirihi sisi wanadamu wachafu; Unachukia upinzani wetu na uasi wetu, hivyo kwa nini Unaishi nasi? Wewe ni Mungu mkuu. Ungeweza kuzaliwa mahali popote, kwa hivyo mbona ilibidi uzaliwe katika nchi hii chafu? Unatuadibu na kutuhukumu kila siku na Unajua wazi kwamba sisi ni uzao wa Moabu, basi kwa nini bado Unaishi kati yetu? Kwa nini Ulizaliwa katika familia ya uzao wa Moabu? Kwa nini Ulifanya hivyo?” Aina hii ya ufahamu wenu inakosa mantiki! Ni aina hii ya kazi tu ambayo inawaruhusu watu kuuona ukuu Wake, unyenyekevu na kujificha Kwake. Yuko tayari kutoa kila kitu kwa ajili ya kazi Yake, na Amevumilia mateso yote kwa ajili ya kazi Yake. Anafanya kwa ajili ya wanadamu, na hata zaidi kumshinda Shetani ili viumbe vyote viweze kutii chini ya utawala Wake. Hii tu ni kazi ya maana, yenye thamani. Kama uzao wa Yakobo ungezaliwa nchini China, katika kipande hiki cha ardhi, na wote walikuwa ninyi nyote, basi umuhimu wa kazi iliyofanyika kwenu ingekuwa nini? Shetani angesema nini? Shetani angesema: “Walikuwa wakikuogopa Wewe, walikutii tangu mwanzo, na hawana historia ya kukusaliti. Wao sio waovu kabisa, wa hali ya chini kabisa, au walio nyuma zaidi kimaendeleo kati ya wanadamu.” Ikiwa inafanyika hivi kwa kweli, nani atakayeridhishwa na kazi hii? Kati ya ulimwengu wote, watu wa Kichina ni watu walio nyuma zaidi kimaendeleo. Wamezaliwa na hali ya chini na uadilifu duni, ni wapumbavu na wenye ganzi, nao ni watovu wa adabu na waliofifia. Wameloweshwa na tabia za kishetani, wachafu na waasherati. Mnayo haya yote. Kwa mintarafu ya tabia hizi potovu, baada ya kazi hii kukamilika watu watazitupilia mbali na wataweza kutii kikamilifu na kufanywa kuwa kamili. Tunda tu kutoka kwa aina hii ya kazi ndilo huitwa ushuhuda kati ya viumbe! Je, unaelewa kile kinachoitwa ushuhuda? Je, ushuhuda unapaswa kutolewaje? Aina hii ya kazi imewafanya kuwa foili pamoja na vyombo vya huduma, na hata zaidi, mmekuwa vyombo vya wokovu. Leo ninyi ni watu wa Mungu na baadaye mtakuwa mifano na vielelezo. Katika kazi hii, mnajitwisha majukumu mbalimbali, na hatimaye mtakuwa vyombo vya wokovu. Watu wengi ni hasi kwa sababu ya hili; Je, si wao ni vipofu kabisa? Huwezi kuona chochote waziwazi! Je, cheo hiki tu kinakuzidi? Je, unaelewa kile kinachotajwa kama tabia ya Mungu yenye haki? Je, unaelewa wokovu wa Mungu ni nini? Je, unaelewa upendo wa Mungu ni nini? Huna uaminifu! Unapotajwa vizuri, unafurahi. Unapotajwa vibaya, hutaki kurudi nyuma. Wewe ni nini? Hufuati njia ya kweli! Afadhali uache kutafuta mara moja. Ni jambo la aibu! Jambo dogo sana linakuzidi. Je, si hii ni ishara ya aibu?

Afadhali uweze kujijua kiasi. Usijione kuwa mkuu sana, wala usiwazie kwenda mbinguni. Tafuta tu kushindwa hapa duniani kwa kufanya wajibu ipasavyo. Usifikiri kuhusu ndoto hizo

zisizo halisi ambazo hazipo! Mtu akisema mambo kama yafuatayo, haya ni maneno kutoka kwa mtu mwenye hamu ya kupata kitu, mwenye ujasiri: “Ingawa mimi ni wa uzao wa Moabu, niko tayari kujitahidi kumpata Mungu, na katika siku zijazo nitamkana babu yangu wa zamani! Alinizaa na pia alinikandamiza, na hadi sasa nimekuwa nikiishi tu katika giza. Leo Mungu ameniachilia na hatimaye nimeiona mbingu. Kupitia kwa ufunuo wa Mungu hatimaye nimeona kwamba mimi ni wa uzao wa Moabu. Awali nilikuwa gizani, na sikujua kwamba Mungu amefanya kazi nyingi sana; yote ni kwa sababu nimepofushwa na Shetani huyu wa zamani. Nitamkana na kumuaibisha kabisa!” Kwa hivyo, mna azma kama hiyo? Licha ya ukweli kwamba nyote mna mfano wa mwanadamu, mnashindwa kustahimili kasi zaidi kuliko mtu mwingine yeyote, nanyi ni wepesi zaidi wa kuathirika kuhusiana na suala hili. Mara tu inapotajwa kwamba ninyi ni uzao wa Moabu, midomo yenu inapinda kwa kuibibidua. Je! Si hii ni tabia ya nguruwe? Haina maana. Mko tayari kutoa dhabihu maisha yenu kwa ajili ya umaarufu na bahati yenu! Huko tayari kuwa uzao wa Moabu, lakini sivyo ulivyo? Ninasema leo kwamba wewe uko hivyo, na lazima ukiri jambo hilo. Siendi kinyume na ukweli. Watu wengine ni hasi kwa sababu ya jambo hili, lakini wewe ni hasi kuhusu nini? Je, si wewe pia ndiye mtoto wa joka kubwa jekundu? Je, ni udhalimu kusema kwamba wewe ni uzao wa Moabu? Angalia kile unachoishi kwa kudhihirisha, ndani na nje. Kutoka kichwani hadi mguuni, hakuna kitu cha kujisifia. Uasherati, uchafu, upofu, upinzani, uasi—si haya yote ni sehemu ya tabia yako? Daima wewe huishi ndani ya nchi ya uasherati nawe hufanya uovu wote. Unadhani kuwa wewe ni mtakatifu wa ajabu sana, lakini hebu yalinganishe mambo ambayo umeyafanya. Unafurahishwa sana na matokeo yako—nini ulicho nacho cha kujisifia? Wewe ni kama mnyama. Huna ubinadamu! Mnaafikiana na wanyama, mnaishi ndani ya uovu, dhana za kiasherati. Je! Mnakosa kiasi gani? Mnakubali kwamba ninyi ni watoto wa joka kubwa jekundu, na mko tayari kufanya huduma, lakini baadaye inaposemekana kuwa wewe ni uzao wa Moabu unakuwa hasi. Je! Si huu ni ukweli? Sawasawa na ulivyojaliwa na mama na baba yako, haijalishi jinsi walivyo wabaya, bado ulizaliwa na wao. Hata ukipata mama wa kambo na kuondoka katika nyumba hiyo, je, si wewe bado ni mtoto wa wazazi wako wa mwanzo? Je! Ukweli huo unaweza kubadilishwa? Je, nimekupachika tu jina la uzao wa Moabu kwa kubahatisha? Watu wengine wanasema: “Je! Si ungenipa tu jina lingine?” Ninasema: “Je, unaonaje Nikikupa jina la foili?” Hawataki kuwa foili pia. Basi unataka kuwa nini? Foili, watendaji huduma—si ninyi mko hivi? Ungechagua nini kingine? Je, si wewe ni mtu aliyezaliwa katika nchi ya joka kubwa jekundu? Haijalishi ni kiasi gani unasema kuwa wewe ni mwana wa Daudi, haikubaliani na ukweli. Je, hili ni jambo ambalo unalichagua wewe mwenyewe? Je, unaweza kuchagua jina lolote zuri unalolipenda kwa ajili yako mwenyewe? Je, ni kweli kuwa watoto wa joka kubwa jekundu waliozungumziwa zamani ni nyinyi. Kuhusu watendaji huduma waliotajwa—je, si wao pia ni nyinyi, watu mliowapotoshwa? Vielelezo vilivyoshindwa, mifano iliyotajwa—si hivi pia ni nyinyi, watu hawa? Njia ya

kukamilishwa—si hilo linasemwa kwa ajili yenu? Wale ambao wanaadibiwa na kuhukumiwa ni nyinyi, na si wale wanaokamilishwa baadaye watakuwa baadhi ya wale miongoni mwenu? Je, jina hili lina maana? Ninyi ni wapumbavu sana kiasi kwamba hamuwezi hata kuona kitu hicho kidogo kwa dhahiri? Hujui nani ni uzao wa nani, lakini Niko dhahiri kulihusu. Nawaambieni. Ikiwa unaweza kulitambua leo hivyo ni vizuri. Usijidhalilishe kila wakati. Zaidi unavyokuwa hasi na kurudi nyuma, ndivyo inavyoonyesha zaidi kwamba wewe ni uzao wa Shetani. Kuna mtu ambaye, unapomtaka asikilize wimbo wa kidini, anasema: “Je, uzao wa Moabu unaweza kusikiza nyimbo za kidini? Sitasikiliza; Mimi sistahili!” Ukimtaka aimbe, anasema: “Ikiwa uzao wa Moabu unaimba, Je, Mungu yuko radhi kusikiliza? Mungu ananichukia. Nina aibu sana kwenda mbele za Mungu na siwezi kushuhudia Kwake. Sitaimba kabisa, Mungu asije akakasirika Anapousikia.” Je! Si hii ni njia hasi ya kulishughulikia? Kama mmoja wa viumbe, ulizaliwa katika nchi ya uasherati na wewe ni mtoto wa joka kubwa jekundu, uzao wa Moabu; unapaswa kumkana babu yako wa zamani na kumkana Shetani wa zamani. Huyu tu ndiye mtu anayemtaka Mungu kwa kweli.

Mwanzoni nilipowapa nafasi ya watu wa Mungu mlikuwa mnaruka juu chini—mliruka kwa furaha zaidi kuliko mtu yeyote. Lakini ilikuwaje mara Niliposema kuwa ninyi ni uzao wa Moabu? Ninyi nyote mlishindwa kustahimili! Ungesema kimo chenu kipo wapi? Dhana yenu ya nafasi ni nzito sana! Wengi hawawezi kujiinua. Wengine huenda kufanya biashara, na wengine huenda kazini. Mara tu Ninaposema kwamba ninyi ni uzao wa Moabu nyote mnataka kukimbia. Je, huku ndiko kushuhudia kwa Mungu ambako huwa mnapigia kelele wakati wote? Je! Shetani ataridhishwa kwa njia hii? Si hii ni alama ya aibu? Ni faida gani kuwa na nyinyi? Ninyi nyote ni taka! Ni mateso ya namna gani ambayo mmestahimili, lakini mnahisi kuwa mmetendewa mabaya sana? Mnafikiri kwamba mara tu Mungu amewatesa hadi kiwango fulani Atafurahi, kana kwamba Mungu alikuja kuwahukumu kimakusudi, na baada ya kuwahukumu na kuwaangamiza, kazi Yake itakuwa imekamilika. Je, ni hivyo ndivyo Nimesema? Je, si hii ni kwa sababu ya upofu wenu? Je! Ni kwamba ninyi wenyewe hamjitahidi kufanya vizuri au kwamba Ninawahukumu kwa makusudi? Sijawahi kufanya hivyo—hilo ni jambo ambalo mlilifikiria wenyewe. Sijafanya kazi kwa njia hiyo kabisa, wala Sina nia hiyo. Kama Ningetaka kuwaangamiza kwa kweli, je, Ningehitaji kuteseka sana hivyo? Ningetaka kuwaangamiza kwa kweli, Ningehitaji kuzungumza nanyi kwa dhati? Mapenzi Yangu ni haya: wakati ambapo Nimewaokoa ndipo Nitakapoweza kupumzika. Zaidi mtu alivyo wa hali ya chini, ndivyo alivyo chombo cha wokovu wangu zaidi. Zaidi mwezavyo kuingia kiutendaji, ndivyo Nitakavyofurahia zaidi. Zaidi mnavyoshindwa kustahimili ndivyo Ninavyofadhaika zaidi. Daima mnataka kuingia kwa mwendo wa furaha kuelekea kiti cha enzi, lakini Nitawaambieni, hiyo sio njia ya kuwaokoa kutokana na uchafu. Njozi ya kukaa kwa kiti cha enzi haiwezi kukufanya kuwa mkamilifu; hiyo

si kweli. Nasema kuwa wewe ni uzao wa Moabu, kisha unakuwa na huzuni. Unasema: “Ikiwa utanifanya niende kuzimu, sitakuwa na ushuhuda Kwako au kuteswa kwa ajili Yako.” Je, si kufanya kwako hivi ni kunipinga Mimi? Je, hili ni la manufaa kwako? Nimekupa neema nyingi sana—umesahau? Umeudharau na kuufedhehesha moyo wa Mungu, ambao ni kama tu wa mama mwenye upendo; matokeo yatakuwa yapi kwako? Sitakulazimisha iwapo hunishuhudii—lakini unapaswa kujua kwamba utaangamizwa mwishowe. Ikiwa Siwezi kupata ushuhuda ndani yako, Nitaupata kwa watu wengine. Hilo halina maana Kwangu, lakini mwishowe utalijutia, na wakati huo utakuwa umeanguka gizani muda mrefu uliopita. Basi nani atakayeweza kukuokoa? Usifikiri kwamba kazi haiwezi kufanyika bila wewe. Hakungekuwa na wengi sana pamoja na wewe, na hakungekuwa na wachache sana bila wewe. Usijione kuwa mheshimiwa sana. Ikiwa hutaki kunifuata, hiyo inaonyesha tu kwamba wewe ni muasi, na hakuna kitu cha kutamanisha ndani yako. Ikiwa wewe ni msemaji mzuri, si hivyo ni kwa sababu tu umejiandaa na maneno Niliyoyaleta kupitia kwa kazi Yangu? Nini ulicho nacho cha kujisifia? Usiruhusu mawazo yako yafikie hitimisho lisilo la msingi! Ikiwa Siwezi kupata utukufu kutoka kwenu, uzao huu wa Moabu, Nitachagua kikundi cha pili, na cha tatu cha uzao wa Moabu kufanya kazi mpaka Nipate utukufu. Ikiwa huko radhi kuwa na ushuhuda Wangu, basi toka nje! Sitakulazimisha! Usifikiri kwamba Nitashindwa kusonga hatua bila ninyi. Kupata vyombo vinavyofaa kwa kazi Yangu katika nchi hii ya China hakuhitaji jitihada. Hakuna kitu kingine chochote kinachoweza kupatikana katika nchi hii—watu wachafu, wapotovu bila shaka wako kila mahali na kazi Yangu inaweza kufanyika popote. Usiwe na kiburi sana! Bila kujali wewe ni mwenye kiburi vipi, je, si bado wewe ni mtoto aliyezaliwa kutokana na uzinzi? Angalia thamani yako, na ni chaguo gani lingine ulilo nalo? Kukukubali tu kuishi ni kuinuliwa kukubwa, kwa hivyo ni nini unajivunia? Kama haingekuwa kwa ajili ya kazi Yangu kukomesha enzi, je, si ungekuwa umeanguka katika majanga ya kawaida na maafa ya kibinadamu zamani sana? Je! Unaweza bado kuishi kwa raha sana? Bado daima unabishana kuhusu suala hili. Tangu Niliposema kwamba wewe ni uzao wa Moabu umekuwa ukibibidua midomo wakati wote. Hufanyi uchunguzi, husomi maneno ya Mungu, na kamwe huwezi kustahimili kuona hili au mtu yule. Unapowaona watu wengine wakielimishwa, unawavuruga na kusema mambo ya kuvunja moyo. Una ujasiri! Unasema: “Uzao wa Moabu una elimu gani? Sitajisumbua.” Je, si hili ni jambo ambalo mnyama angesema? Je, hata unafikiriwa kuwa mwanadamu? Nimesema mambo mengi kwako, lakini haijafanikisha chochote. Je, Nimefanya kazi hii yote bure? Je, Nimesema maneno haya yote bure? Hata mbwa anaweza kutikisa mkia wake; mtu kama huyu hata si mzuri kama mbwa! Je, unastahili kuitwa mwanadamu? Ninaponena kuhusu uzao wa Moabu, watu wengine hujishusha hadhi kimakusudi. Wanavaa tofauti kuliko hapo awali nao ni wachafu sana kisai kwamba hawaonekani kama watu, nao hunung’unika: “Mimi ni uzao wa Moabu. Sifai kitu. Ni njozi kufikiria kuhusu kupata baraka zozote. Je, uzao wa Moabu unaweza kufanywa kuwa mkamilifu?” Mara tu Ninaponena kuhusu

uzao wa Moabu, watu wengi hawana matumaini tena, na kusema: “Mungu anasema kwamba sisi ni uzao wa Moabu—hii inaonyesha nini? Angalia sauti Anayotumia—haibadiliki! Hakuna upendo katika maneno Yake. Je! Si sisi ni malengo ya maangamizo?” Je! Umesahau kile kilichosemwa hapo awali? Leo neno “uzao wa Moabu” ni jambo pekee ambalo umekumbuka? Kwa kweli, maneno mengi ni kwa ajili ya kufikia kitu, lakini pia yanafichua ukweli wa mambo. Watu wengi hawaliadini. Huko tayari kuteseka kwa njia hiyo kwa ajili Yangu. Unaogopa kifo na daima unataka kutoroka. Ikiwa unataka kwenda Sitakulazimisha kukaa, lakini ni lazima Nikweleze wazi jambo moja: Usiishi maisha yote bure, na usisahau mambo yote Nilivyokwambia zamani. Kama mmoja wa viumbe unapaswa kutekeleza wajibu wa mmoja wa viumbe. Usifanye mambo dhidi ya dhamiri yako; unachopaswa kufanya ni kujitolea kwa Bwana wa uumbaji. Uzao wa Moabu pia ni viumbe walioumbwa, ni jinsi tu wao ni foili^[a] na wamelaaniwa. Chochote kitokeacho, bado wewe ni mmoja wa viumbe. Hujakosea sana ukisema hili: “Ingawa mimi ni uzao wa Moabu, nimefurahia neema nyingi ya Mungu mbeleni, hivyo ni lazima niwe na dhamiri. Nitakiri tu lakini sitafikiri sana kulihusu. Hata kama nitateseka ndani ya mkondo huu, nitateseka mpaka mwisho. Kama mimi ni wa uzao wa Moabu basi iwe hivyo. Bado nitafuata hadi mwisho!” Lazima ufuata mpaka mwisho. Ukikimbia kwa kweli huna matumaini ya baadaye—umeingia kwenye barabara ya maangamizo.

Ni vizuri kuwafanya muelewe asili yenu, na kuwafanya muuelewe ukweli wa mambo ni wenye manufaa kwa kazi. Vinginevyo, matokeo ambayo yanapaswa kufanikishwa hayatafanikishwa. Hii ni sehemu ya kazi ya kushinda, na ni hatua muhimu katika kazi. Huo ni ukweli. Kufanya kazi hii ni kuziamsha roho za watu, kuamsha hisia za dhamiri zao na kuwaruhusu watu kupata wokovu huu mkubwa. Ikiwa mtu ana dhamiri, anapaswa kumshukuru Mungu hata zaidi anapoona kwamba yeye ni wa hadhi. Anapaswa kuyashikilia maneno Yake mikononi mwake, ashikilie kwa nguvu neema ambayo Amempa, na hata alie kwa uchungu na kusema: “Nafasi yetu ni ya chini sana na hatujapata chochote duniani. Hakuna mtu kutuheshimu, watu hawa wa hali ya chini. Tunateswa katika mazingira yetu ya nyumbani, waume zetu hutukana, wake zetu hutushutumu, watoto wetu hutudharau, na tunapokuwa wazee, binti zetu wakwe pia hututesa. Hakika hatujateseka kidogo, na kwamba sasa tunafurahia upendo mkuu wa Mungu ni furaha sana! Kama haungekuwa wokovu wa Mungu kwetu, tungewezaje kung’amua mateso ya kibinadamu vizuri? Je, si bado tungekuwa tunapotoka katika dhambi hii? Je, huku si Mungu kutuiniua? Mimi ni mmoja wa watu duni kabisa, na Mungu ameniinua juu sana. Hata kama nitaangamia bado lazima niulipize upendo Wake. Mungu anatumshukuru na Anazungumza nasi, sisi watu duni mno, uso kwa uso nasi. Anauchukua mkono wangu kunifunza. Kwa kinywa Chake, Ananilisha. Anaishi nami na kuteseka nami. Hata anaponiadibu—ninaweza kusema nini? Je, si kuadibiwa pia ni kuinuliwa na Mungu? Nimeadibiwa lakini naweza kuona haki Yake.

Lazima niulipize upendo wa Mungu. Siwezi kuasi dhidi ya Mungu tena.” Nafasi ya Mungu na hadhi Yake si sawa na ya watu, lakini mateso Yake ni sawa, na kile Anachokula na kuvaa ni sawa, ni watu wote tu humheshimu—hii ndiyo tofauti pekee. Je, si kila kitu kingine ambacho kinafurahiwa ni sawa? Hivyo, nini kinawapa haki ya kumwomba Mungu awatendee kwa namna fulani? Mungu amevumilia mateso makubwa mno na kufanya kazi kubwa sana, na nyinyi—mlio chini kuliko mchwa, kuliko wadudu—mmepata kuinuliwa pakubwa leo. Ikiwa huwezi kuulipiza upendo wa Mungu, dhamiri yako iko wapi? Watu wengine hunena kutoka mioyoni mwao na kusema: “Kila wakati nikifikiri kuondoka kutoka kwa Mungu macho yangu yanajawa na machozi nami nahisi kuhukumiwa na dhamiri yangu. Mimi ni mwenye kuwiwa kwa Mungu. Siwezi kufanya hivi. Siwezi kuwa namna hiyo Kwake. Ningekufa na kufa kwangu kuipe kazi Yake utukufu, nitaridhika kupita kiasi. Vinginevyo, hata nikiishi sitahisi amani.” Sikiliza maneno haya—yanaelezea wajibu ambao kiumbe aliyeumbwa anapaswa kutimiza. Ikiwa mtu anakuwa na maono haya ndani yake kila mara, atahisi kuwa dhahiri na starehe ndani yake; atakuwa na uhakika wa mambo haya. Utasema: “Mungu haniumizi na Hanifedheheshi kimakusudi wala Haniaibishi. Ingawa Ananena kwa ukali kwa kiasi fulani na huuchoma moyo, ni kwa ajili yangu mwenyewe. Ingawa Ananena kwa ukali namna hiyo, bado Ananiokoa, na Yeye bado ni mwenye huruma kwa udhaifu wangu. Hanihukumu na ukweli. Naamini kwamba Mungu ni wokovu.” Ikiwa kweli una maono haya, uwezekano wa wewe kutoroka utakuwa mdogo. Dhamira yako haitakuruhusu uende, na shutuma yake itakuambia kwamba hupaswi kumtendea Mungu kwa namna hiyo. Unafikiri kuhusu neema yote uliyoipata, maneno yote ambayo umeyasikia—je, unaweza kuyasikiliza bure? Haijalishi ni nani anakimbia, wewe huwezi. Watu wengine hawaamini, lakini lazima wewe uamini. Watu wengine wanamtelekeza Mungu, lakini lazima wewe umtete Mungu na kushuhudia Kwake. Wengine humkashifu Mungu, lakini wewe huwezi. Haijalishi jinsi Mungu asivyo na huruma kwako, bado unapaswa kumtendea vyema. Unapaswa kuulipiza upendo Wake na lazima uwe na dhamiri, kwa sababu Mungu hana hatia. Kuja Kwake duniani kutoka mbinguni kufanya kazi miongoni mwa wanadamu kulikuwa aibu kubwa tayari. Yeye ni mtakatifu bila uchafu hata kidogo. Kuja kwenye nchi ya uchafu—ni fedheha kiasi gani ambayo Amevumilia? Kufanya kazi ndani yenu ni kwa ajili yenu. Ikiwa huna dhamiri katika kumtendea Yeye, ingekuwa bora kufa kifo cha mapema!

Hivi sasa, watu wengi wanakosa kipengele hiki cha maono na hawawezi kabisa kuielewa kazi hii na hawajui nini Mungu anataka hasa kukamilisha kupitia kazi hii. Hasa wale waliokanganyika—ni kama wameingia katika matata mengi na kutunduwazwa baada ya zamu chache. Ukifafanua kikamilifu lengo la mpango wa usimamizi wa Mungu kwao, hawatakanganyikiwa. Watu wengi hawawezi kulielewa, na wanaamini kwamba kazi ya Mungu ni kuwatesa watu. Hawaelewi hekima na maajabu ya kazi Yake, na hawaelewi kwamba kazi

Yake ni kufichua nguvu Yake kuu, na hata zaidi ni kuwaokoa wanadamu. Hawaoni yote hayo, wao huona tu kama wana matumaini yoyote, na kama wataweza kuingia mbinguni. Wanasema: “Kazi ya Mungu daima ni ya mzunguko; kama ungetufanya tu tuione hekima Yako moja kwa moja hiyo ingekuwa vizuri. Hupaswi kututesa kwa njia hii. Tunakosa sana katika ubora wa tabia na hatuyafahamu mapenzi Yako. Ingekuwa vizuri sana kama Ungenena na kutenda tu moja kwa moja. Unatufanya tukisie, lakini hatuwezi. Ingekuwa vizuri kama Ungeharakisha na kuturuhusu tuuone utukufu Wako. Nini haja ya kufanya mambo kwa njia ya mzunguko?” Kile mnachokosa sana sasa ni dhamiri. Zingatieni hili zaidi na fungueni macho yenu wazi kabisa ili muone nani hasa anayefanya hatua kwa hatua kwa kazi. Msifikie uamuzi upesi bila kutafakari. Sasa umeelewa zaidi kwa juujuu njia ya maisha unayopaswa kupitia. Bado kuna kiasi kikubwa cha ukweli ambacho unapaswa kupitia, na siku inapokuja ambapo unaweza kuuelewa kikamilifu, hutasema hivyo tena, wala hutalalamika. Wala hutaufafanua bila uzito. Utasema: “Mungu ni mwenye busara sana, mtakatifu sana. Yeye ni mwenye nguvu sana!”

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Matukio Aliyopitia Petro: Ufahamu Wake wa Adabu na Hukumu

Alipokuwa akiadibiwa na Mungu, Petro aliomba, “Ee Mungu! Mwili wangu ni mkaidi, na unaniadibu na kunihukumu mimi. Nafurahi katika adabu Yako na hukumu, na hata kama Hunitaki mimi, katika hukumu Yako mimi ninaona tabia Yako takatifu na tabia Yako ya haki. Unaponihukumu, ili wengine wapate kuiona hali Yako ya haki katika hukumu Yako, ninaridhika. Ikiwa inaweza kuionyesha tabia Yako na kuiruhusu tabia Yako ya haki iweze kuonekana na viumbe wote, na kama inaweza kuufanya upendo wangu Kwako uwe safi zaidi, kwamba naweza kufikia mfano wa yule ambaye ni mwenye haki, basi hukumu Yako ni nzuri, kwa maana hivyo ndivyo mapenzi Yako ya neema yalivyo. Najua kwamba bado kuna mengi ndani yangu yaliyo ya uasi, na kwamba mimi bado sifai kuja mbele Yako. Ningependa unihukumu hata zaidi, iwe ni kupitia mazingira ya uhasama au mateso makubwa; haijalishi ni nini Utakayofanya, kwangu ni ya thamani. Upendo Wako ni mkuu, na mimi niko tayari kujiweka katika huruma Yako bila malalamiko hata kidogo.” Huu ni ufahamu wa Petro baada ya yeye kuiona kazi ya Mungu, na pia ni ushahidi wa upendo wake kwa Mungu. Leo hii, nyinyi tayari mmeshashindwa—lakini ni jinsi gani ushindi huu unaonekana ndani yenu? Baadhi ya watu wanasema, “Ushindi Wangu ni neema kuu na kuinuliwa kwa Mungu. Ni sasa tu ndipo ninapotambua kwamba maisha ya mwanadamu ni bure na yasiyo na maana. Mwanadamu hutumia maisha yake kukimbia huku na kule, kuzalisha na kuongeza kizazi baada ya kizazi cha

watoto, na hatimaye huwachwa bila chochote. Leo, baada tu ya kushindwa na Mungu ndio nimeona kwamba hakuna thamani ya kuishi kwa njia hii; kwa kweli ni maisha yasiyo na maana. Afadhali nife na kuyasahau haya!” Je, watu kama hao ambao wameshindwa wanaweza kukombolewa na Mungu? Je, wanaweza kuwa vielelezo na mifano? Watu kama hao ni somo katika kutoshughulika, hawana matarajio, na wala kujitahidi kujiboresha wenyewe! Ingawa wao huhesabiwa kama walioshindwa na Mungu, watu kama hao wasioshughulika hawawezi kufanywa wakamilifu. Karibu mwishoni mwa maisha yake, baada ya yeye kufanywa kuwa mkamilifu, Petro akasema, “Ee Mungu! Kama ningeweza kuishi miaka michache zaidi ya hapa, ningependa kufikia usafi zaidi na upendo wa ndani Kwako.” Alipokuwa karibu kusulubiwa, katika moyo wake akaomba, “Ee Mungu! Wakati Wako umewadia, wakati ulionitayarishia umefika. Mimi lazima nisulubiwe kwa ajili Yako, lazima niwe na ushuhuda huu Kwako, na ninatumai kwamba upendo wangu utaweza kukidhi mahitaji Yako, na kwamba unaweza kuwa safi zaidi. Leo, kuwa na uwezo wa kufa kwa ajili Yako, na kusulubiwa kwa ajili Yako, ni faraja na ya kutia moyo kwangu, kwa maana hakuna kinachonifurahisha kuliko kuweza kusulubiwa kwa ajili Yako na kukidhi matakwa Yako, na kuweza kujitoa Kwako, kutoa maisha yangu Kwako. Ee Mungu! Wewe ni wa kupendeza kweli! Kama Ungeniruhusu niishi, ningenuia kukupenda zaidi. Mradi tu ninaishi, mimi nitakupenda. Natamani kukupenda kwa undani zaidi. Unanihukumu, Unaniadibu, na kunijaribu kwa sababu mimi si mwenye haki, kwa sababu nimetenda dhambi. Na tabia Yako ya haki inakuwa dhahiri zaidi kwangu. Hii ni baraka kwangu, kwa maana ninapata uwezo wa kukupenda kwa undani zaidi, na mimi niko tayari kukupenda kwa njia hii hata kama Hunipendi. Mimi niko tayari kutazama tabia Yako ya haki, kwa maana inafanya niweze kuishi maisha ya maana zaidi. Mimi ninahisi kwamba maisha yangu sasa ni ya maana zaidi, kwa maana nimesulubiwa kwa ajili Yako, na ni jambo la maana kufa kwa ajili Yako. Hata hivyo bado mimi sijaridhika, kwa maana najua kidogo sana kukuhusu, najua kwamba siwezi kutimiza matakwa Yako kikamilifu, na kuwa nimekulipa kidogo mno. Katika maisha yangu, sijaweza kurudisha nafsi yangu Kwako kikamilifu; Niko mbali sana na hili. Nikitazama nyuma kwa wakati huu, mimi huhisi kuwa nina mzigo mkubwa wa madeni kwako, na sina muda mwingine ila huu kwa ajili ya kurekebisha makosa yangu na upendo wote ambao sijakulipa Wewe.”

Mwanadamu lazima azingatie kuishi kwa kudhihirisha maisha ya maana, na hapaswi kuridhika na hali yake ya sasa. Kuishi kama mfano wa Petro, lazima awe na maarifa na uzoefu wa Petro. Mtu lazima ashikilie mambo ambayo ni ya juu na zaidi ya yaliyo makuu. Ni lazima yeye afuatilie kwa ndani zaidi, usafi zaidi wa upendo wa Mungu, na maisha ambayo yana thamani na umuhimu. Haya tu ndiyo maisha; hivi tu ndivyo mwanadamu atakuwa sawa na Petro. Lazima kuzingatia kuwa makini kwa kuingia kwako kwa upande mwema, na lazima uhakikishe

kwamba haurudi nyuma kwa ajili ya urahisi wa kitambo na kupuuza mambo mengine makubwa, zaidi maalum, na zaidi kwa ukweli wa vitendo. Upendo wako lazima uwe wa vitendo, na lazima utafute njia ya kujitoa katika upotovu huu, maisha yasiyo na kujali ambayo hayana tofauti na ya mnyama. Lazima uishi maisha ya maana, maisha ya thamani, na usijipumbaze, au kufanya maisha yako kama kitu cha kuchezea. Kwa kila mtu ambaye anatumai kumpenda Mungu, hakuna ukweli usioweza kupatikana, na hakuna haki wasioweza kusimama imara nayo. Unafaa kuishije maisha Yako? Unapaswa kumpenda Mungu vipi na kutumia upendo huu ili kukidhi hamu Yake? Hakuna kubwa zaidi katika maisha Yako. Zaidi ya yote, lazima uwe na matarajio hayo na uvumilivu, na hupaswi kuwa kama wanyonge wasio na nia. Lazima ujifunze jinsi ya kupitia maisha ya maana, na kuuona ukweli wa maana, na hupaswi kujichukua kipurukushani katika njia hiyo. Bila wewe kujua, maisha Yako yatakupita tu; na baada ya hapo, je utakuwa una fursa nyingine ya kumpenda Mungu? Je, mwanadamu anaweza kumpenda Mungu baada ya kufa? Lazima uwe na matarajio na dhamiri sawa na ya Petro; maisha Yako ni lazima yawe na maana, na usifanye mchezo na nafsi yako. Kama mwanadamu, na kama mtu ambaye anamfuata Mungu, ni lazima uweze kufikiria kwa makini jinsi unavyoendesha maisha yako, jinsi unapaswa kujitoa mwenyewe kwa Mungu, jinsi unapaswa kuwa na imani yenye maana zaidi katika Mungu, na jinsi, kwa kuwa wewe unampenda Mungu, unapaswa kumpenda Yeye kwa njia ambayo ni safi zaidi, nzuri zaidi, na bora zaidi. Leo hii, huwezi tu kuridhika na jinsi wewe umeshindwa, lakini lazima pia uzingatie njia ambayo utatembelea siku zijazo. Lazima uwe na matarajio na ujasiri wa kufanywa mkamilifu, na hupaswi daima kufikiria kwamba huwezi. Je, ukweli una maonevu? Je, ukweli huwapinga watu kwa makusudi? Kama wewe utafuata ukweli, je unaweza kukushinda? Kama wewe utasimama imara kwa ajili ya haki, je utakuangusha chini? Kama ni hamu yako kwa kweli kufuata maisha, je, maisha yanaweza kukuhepa? Kama wewe huna ukweli, si kwamba ukweli unakupuuza, lakini ni kwa sababu wewe unakaa mbali na ukweli; kama huwezi kusimama imara kwa ajili ya haki, hiyo si kwa sababu kuna kitu kibaya na haki, lakini ni kwa sababu unaamini kuwa ni kinyume na ukweli; kama hujapata maisha baada ya kuyatafuta kwa miaka mingi, si kwa sababu maisha hayana dhamira kwako, bali ni kwa sababu wewe huna dhamira kwa maisha, na kuwa umeyafukuzilia mbali maisha; Iwapo unaishi katika mwanga, na hujaweza kuupata mwanga, hiyo siyo kwa sababu mwanga hauwezi kukuangazia, lakini kwa sababu wewe hujaweka makini kwa kuwepo kwa mwanga, na hivyo mwanga umeondoka kwa kimya. Kama huwezi kufuata, basi inaweza kusemwa kwamba wewe ni taka usiye na maana, na huna ujasiri katika maisha yako, na huna roho ya kupinga nguvu za giza. Wewe ni mdhaifu mno! Huwezi kutoroka nguvu za Shetani ambazo zimekuzingira, na kuwa uko tayari tu kuishi haya maisha ya usalama na kufa katika ujinga. Kile unachopaswa kufanya ni kutekeleza azma yako ya kuwa mshinde; huu ni wajibu wako uliokushikilia. Kama wewe umeridhika na kushindwa, basi unafukuza kuwepo kwa mwanga. Lazima uvumilie mateso kwa

ajili ya ukweli, lazima ujitoe kwa ajili ya ukweli, lazima uvumilie udhalilishaji kwa ajili ya ukweli, na kupata ukweli zaidi lazima upate mateso zaidi. Hili ndilo unalopaswa kufanya. Msitupilie mbali ukweli kwa ajili ya maisha ya amani ya familia, na lazima msiipoteze heshima na uadilifu wa maisha kwa ajili ya starehe ya muda mfupi. Unapaswa kufuata yote ambayo ni ya kupendeza na mema, na unapaswa kufuatilia njia katika maisha ambayo ni ya maana zaidi. Kama wewe unaishi maisha ya kishenzi, na wala hufuati malengo yoyote, je, si huko ni kupoteza maisha Yako? Ni nini unachoweza kupata kutoka kwa maisha ya aina hii? Unapaswa kuziacha starehe zote za mwili kwa ajili ya ukweli mmoja, na hupaswi kutupilia mbali ukweli wote kwa ajili ya starehe ya muda mfupi. Watu kama hawa hawana uadilifu au heshima; hakuna maana ya kuwepo kwao!

Mungu humuadibu na kumhukumu mwanadamu kwa sababu inatakiwa vile na kazi Yake, na zaidi ya hayo, kwa sababu yanahitajika na mwanadamu. Mwanadamu anahitaji kuadibiwa na kuhukumiwa, na ni vile tu ndivyo anaweza kufikia upendo wa Mungu. Leo, mmeshawishiwa kikamilifu, lakini wakati mnapokutana na kizingiti kidogo mtakuwa mashakani; kimo chenu bado ni kidogo mno, na nyinyi bado mnahitaji kupata adabu na hukumu hiyo zaidi ili mfikie ufahamu zaidi. Leo, mna heshima kidogo kwa Mungu, na mnamcha Mungu, na mnajua Yeye ni Mungu wa kweli, lakini hamna upendo mkubwa wa Kwake, na bado hamjafikia upendo safi; maarifa yenu ni ya juujuu, na kimo chenu bado hakitoshi. Wakati nyinyi mnapatana na mazingira, bado hamjashuhudia, sehemu ndogo ya kuingia kwenu ndiyo makini, na nyinyi hamjui jinsi ya kufanya mazoezi. Watu wengi ni watazamaji tu na si watendaji; wao humpenda Mungu tu kwa siri katika nyoyo zao, lakini hawana njia ya mazoezi, wala hawafahamu vizuri malengo yao ni nini. Wale ambao wamefanywa wakamilifu hawana tu ubinadamu wa kawaida, lakini wanao ukweli unaozidi vipimo vya dhamiri, na kwamba ni kuu zaidi kuliko viwango ya dhamiri; wao hawatumi tu dhamiri yao kulipia upendo wa Mungu, lakini, zaidi ya hayo, wanajua Mungu, na wameona kwamba Mungu ni mzuri, na Anastahili upendo wa mtu, na kwamba kuna mambo mengi ya upendo katika Mungu ambayo mtu hana budi ila kumpenda Mungu. Upendo kwa Mungu wa wale ambao wamekuwa wakamilifu ni kwa ajili ya kutimiza matarajio yao binafsi. Upendo wao ni wa papo hapo, upendo usiouliza chochote, na usio wa kubadilisha na kitu. Wanampenda Mungu kwa sababu ya ufahamu wao Kwake, na sio kwa sababu nyingine. Watu kama hawa hawajali kama Mungu anawapa neema au la, wanaridhishwa na kumridhisha Mungu. Hawabishani na Mungu wapate kitu kwa badala yake, wala kupima upendo wao kwa Mungu na dhamiri: Umenipa, kwa hivyo nitakupenda kwa badala yake; kama Wewe Hunipi, basi sina chochote cha kukupa kwa badala yake. Wale ambao wamekuwa wakamilifu daima huamini kwamba: Mungu ni Muumba, na Yeye hufanya kazi Yake juu yetu. Kwa vile nina fursa hii, hali, na uwezo wa kufanywa kamili, azma yangu inafaa kuwa kuishi kwa

kudhihirisha maisha yaliyo na maana, na ninapaswa kumridhisha Yeye. Ni kama yale aliyopitia Petro: Alipokuwa katika hatua ya udhaifu, alisali kwa Mungu na kusema, “Ee Mungu! Bila kujali wakati au mahali, Unajua kuwa mimi daima hukukumbuka. Haijalishi wakati au mahali, Unajua kuwa mimi nataka kukupenda, lakini kimo changu ni kidogo mno, mimi ni mdhaifu mno na sina nguvu, upendo wangu ni mdogo sana, na uaminifu wangu kwako pia mdogo. Ikilinganishwa na upendo Wako, mimi sifai kuishi. Natamani tu kwamba maisha yangu yasiwe bure, na kwamba nisiweze tu kulipa upendo wako, lakini, kwamba niweze kukukabidhi vyote nilivyo navyo. Kama naweza kukuridhisha, basi kama kiumbe, mimi nitakuwa na amani moyoni, na sitauliza chochote zaidi. Ingawa mimi ni mdhaifu na asiye na nguvu sasa, siwezi kusahau ushauri Wako, na siwezi kusahau upendo Wako. Sasa sifanyi kitu chochote zaidi ya kulipa upendo wako. Ee Mungu, ninahisi kuwa mbaya! Ninawezaje kukupa upendo ulio moyoni mwangu, nitafanyaje yote ninayoweza, na niwe na uwezo wa kutimiza matakwa Yako, na kuwa na uwezo wa kukupa kila nilicho nacho? Unajua udhaifu wa mwanadamu; ninawezaje kuustahili upendo wako? Ee Mungu! Unajua mimi ni wa kimo kidogo, kwamba upendo wangu pia ni mdogo. Jinsi gani niweze kufanya jinsi niwezavyo katika aina hii ya mazingira? Ninajua napaswa kuulipa upendo Wako, najua kwamba napaswa kutoa yote niliyo nayo Kwako, lakini leo kimo changu ni kidogo mno. Naomba kwamba Wewe Unipe nguvu, na kunipa ujasiri, ili niweze kuwa na upendo safi zaidi na kujitoa kwa ajili Yako, na niweze kutoa yote niliyo nayo Kwako; sitaweza kuulipa upendo Wako tu, lakini zaidi nitaweza kupitia adabu Yako, hukumu na majaribu, na hata laana kali zaidi. Umeniruhusu kutazama upendo wako, na sina uwezo wa kutokukupenda Wewe, na ingawa mimi ni mdhaifu na asiye na nguvu leo, inawezekanaje nikusahau Wewe? Upendo wako, adabu na hukumu imenisababisha mimi kujua Wewe, lakini nahisi sina uwezo wa kutimiza upendo Wako kwa hakika, kwa maana Wewe ni Mkuu zaidi. Nitawezaje kutoa yote niliyo nayo kwa Muumba?” Hilo ndilo lilikuwa ombi la Petro, ilhali kimo chake kilikuwa duni. Wakati huu, alijisikia kama kisu kilikuwa kinasukumwa katika moyo wake na alikuwa katika maumivu makali; hakujua cha kufanya katika hali hiyo. Hata hivyo bado aliendelea kuomba: “Ee Mungu! Mwanadamu ni wa kimo cha kitoto, dhamiri yake ni dhaifu, na kitu tu naweza kufikia ni kurejesha upendo Wako. Leo, mimi sijui jinsi ya kukidhi matamano Yako, na ningependa tu kufanya yote ninayoweza, kutoa yote niliyo nayo, na kukukabidhi Wewe yote niliyo nayo. Licha ya Hukumu Yako, licha ya adabu Yako, licha ya yote uliyonipa, licha ya yale Unachukua kutoka kwangu, Niokoe kutokana na aina yoyote ya lalamiko Kwako kutoka kwangu. Mara nyingi, wakati uliniadibu na kunihukumu, nilijinung’unikia, na sikuwa na uwezo wa kufikia usafi, au wa kutimiza matakwa Yako. Ulipaji wangu wa upendo Wako ulizaliwa kutokana na lazima, na katika wakati huu najichukia hata zaidi.” Ilikuwa ni kwa sababu yeye alitaka upendo safi zaidi wa Mungu kwamba Petro aliomba kwa njia hii. Alikuwa akitafuta, na kumwomba, na, zaidi ya hayo, alikuwa akiishtaki nafsi yake, na kukiri dhambi zake kwa Mungu.

Alijisikia mdeni kwa Mungu, na aliichukia nafsi yake, ilhali alikuwa pia kwa kiasi fulani mwenye huzuni na asiyesughulika. Yeye daima aliona hivyo, kama kwamba hakuwa mzuri wa kutosha kwa ajili ya matakwa ya Mungu, na kuwa hakuweza kufanya bora zaidi. Katika hali kama hiyo, Petro bado alifuata imani ya Ayubu. Aliona jinsi imani ya Ayubu ilivyokuwa kubwa, kwa maana Ayubu aliona kwamba yote yalifanywa na Mungu, na ilikuwa ni ya asili ya Mungu kuchukua kila kitu kutoka kwake, na kwamba Mungu angempa yeyote ambaye Angependa kumpa—hivyo ndivyo ilivyokuwa tabia ya haki ya Mungu. Ayubu hakuwa na malalamiko, na bado aliweza kumtukuza Mungu. Petro pia alijua mwenyewe, na katika moyo wake akaomba, “Leo mimi siwezi kuridhika na kulipa upendo Wako kwa kutumia dhamiri yangu na kwa upendo wowote ninaokupa, kwa sababu mawazo yangu yamepotoshwa sana, na kwa sababu mimi sina uwezo wa kukuona Wewe kama Muumba. Kwa sababu mimi bado sifai kukupenda, lazima kukamilisha uwezo wa kutoa yote niliyonayo Kwako, na hivyo nitafanya kwa hiari. Ni lazima nijue yote Uliyofanya, na sina budi, na mimi lazima nitazame upendo Wako, na kuwa na uwezo wa kusema sifa Zako, na kutaja jina lako takatifu, ili Uweze kupata utukufu mwingi kupitia kwangu. Mimi niko tayari kusimama imara katika ushuhuda huu Kwako. Ee Mungu! Upendo wako ni wenye thamani na wa kupendeza; jinsi gani mimi ningetaka kuishi katika mikono ya yule mwovu? Je, mimi sikuumbwa na Wewe? Ningewezaje kuishi chini ya miliki ya Shetani? Ningependa nafsi yangu nzima iishi chini ya adabu Yako. Sitaki kuishi chini ya miliki ya yule mwovu. Kama mimi ninaweza kutakaswa, na ninaweza kutoa yote niliyonayo Kwako, mimi niko tayari kutoa mwili wangu na akili kwa hukumu na adabu Yako, kwa maana mimi nachukizwa na Shetani, na sina nia ya kuishi chini ya uwanja wake. Kupitia hukumu Yako kwangu, umenionyesha tabia Yako ya haki; Nina furaha, na sina malalamiko hata kidogo. Kama mimi nina uwezo wa kutekeleza jukumu la kiumbe, mimi niko tayari kuwa maisha yangu yote yaambatane na hukumu Yako, kwa njia ambayo mimi nitapata kujua tabia Yako ya haki, na kujiondolea ushawishi wa yule mwovu.” Petro aliomba hivyo kila mara, na daima alitafuta hivyo, na aliufikia ulimwengu wa juu, kwa ulinganisho. Hakuweza tu kuulipa upendo wa Mungu, lakini, la muhimu zaidi, yeye alitimiza wajibu wake kama kiumbe. Hakutuhumiwa tu na dhamiri yake, lakini alikuwa pia na uwezo wa kuvuka viwango vya dhamiri. Maombi yake yaliendelea kwenda mbele za Mungu, hivyo kwamba matarajio yake yalikuwa milele juu, na upendo wake kwa Mungu ulikuwa milele mkuu. Ingawa yeye alipitia maumivu makali, bado hakusahau kumpenda Mungu, na bado alitaka kufikia uwezo wa kuelewa mapenzi ya Mungu. Kwa maombi yake yalitamkwa maneno yafuatayo: Sijatimiza chochote zaidi ya ulipaji wa upendo wako. Sijatoa ushuhuda Kwako mbele ya Shetani, sijajiweka huru mwenyewe kutokana na ushawishi wa Shetani, na bado naishi miongoni mwa umbo la mwili. Ningependa kutumia upendo wangu kumshinda shetani, na kumwaibisha, na hivyo kuridhisha hamu Yako. Ningependa kujitoa mzima Kwako, nisijitoe hata kidogo kwa Shetani, kwani Shetani ni adui

Wako. Zaidi ya alivyoendelea kwa njia hii, ndivyo alivyo zidi kusongeshwa, na ndivyo ujuzi wake wa mambo haya ulivyo zidi kukua. Bila kujua, alitambua kwamba anapaswa kujikwamua kutokana na ushawishi wa Shetani, na kujirudisha mwenyewe kabisa kwa Mungu. Huo ndio ulimwengu alioufikia. Alikuwa anauzidi kwa mbali ushawishi wa Shetani, na kujitoa mwenyewe kwenye raha na starehe za mwili, na alikuwa tayari kupitia kwa kina zaidi adabu zote na hukumu ya Mungu. Alisema, “Hata ingawa ninaishi katika adabu Yako, na huku kukiwa na hukumu Yako, bila kujali ugumu unaohusiana na maisha, bado mimi sina nia ya kuishi chini ya miliki ya Shetani, sina nia ya kuteseka na hila za Shetani. Mimi nina furaha kuishi kwenye laana Yako, na ninapata uchungu kwa kuishi katika baraka za shetani. Nakupenda kwa kuishi katika hukumu Yako, na hii huniletea furaha kuu. Adabu Yako na hukumu ni yenye uadilifu na takatifu; ni vyema ukinitakasa, na hata zaidi kuniokoa. Ninapenda niishi maisha yangu yote katika hukumu Yako na kuwa chini ya uchungaji Wako. Sina nia ya kuishi chini ya mamlaka ya Shetani hata kwa dakika moja; Napenda kutakaswa na Wewe; hata kama ninapitia taabu, sina nia ya kutumiwa na kuhadaiwa na shetani. Mimi, kiumbe hiki, nafaa nitumike na Wewe, nijazwe na Wewe, nihukumiwe na Wewe, na kuadibiwa na Wewe. Nafaa hata nipokee laana kutoka Kwako. Moyo wangu hufurahi wakati Uko tayari kunibariki, kwa maana nimeona upendo Wako. Wewe ni Muumba, na mimi ni kiumbe: Sifai kukusaliti Wewe na kuishi chini ya himaya ya Shetani, wala sifai kutumiwa na Shetani. Mimi nafaa kuwa farasi wako, au ng’ombe, badala ya kuishi kwa ajili ya Shetani. Afadhali niishi katika adabu Yako, bila neema ya kimwili, na hii itanipa raha na starehe hata kama ningepoteza neema Yako. Ingawa neema Yako haiko nami, mimi nafurahia kuadibiwa na kuhukumiwa na Wewe; Hii ndiyo baraka Yako nzuri zaidi, neema Yako kuu. Ingawa Wewe daima ni Mkuu na mwenye ghadhabu kwangu, bado mimi siwezi kukuacha, bado sina uwezo wa kukupenda vya kutosha. Ningependelea kuishi katika nyumba Yako, Ningependa kulaaniwa, kuadibiwa, na kuchapwa na Wewe, na sina nia ya kuishi chini ya himaya ya Shetani, wala mimi sina nia ya kukimbilia na kushughulika kwa ajili ya mwili tu, zaidi ya hayo siko tayari kuishi kwa ajili ya mwili.” Upendo wa Petro ulikuwa upendo safi. Huu ni ujuzi wa kufanywa mkamilifu, na ni ulimwengu wa juu wa kufanywa mkamilifu, na hakuna maisha yaliyo na maana zaidi ya haya. Alikubali adabu ya Mungu na hukumu, aliipenda tabia ya Mungu ya haki, na hakuna jambo kuhusu Petro lililokuwa la thamani zaidi ya hili. Alisema, “Shetani ananipa starehe za mwili, lakini mimi sithamini hayo. Adabu ya Mungu na hukumu inakuja juu yangu—na katika hili mimi nimeneemeka, katika hili mimi ninapata starehe, na katika hili mimi nimebarikiwa. Kama si kwa hukumu Yake, mimi singeweza kumpenda Mungu, bado ningeishi chini ya himaya ya Shetani, bado ningedhibitiwa nayo, na ningekuwa naamuriwa nayo. Kama ingekuwa vile, singewahi kuwa binadamu wa kweli, kwa maana singeweza kumtoshleza Mungu, na singejitoa kikamilifu kwa Mungu. Japokuwa Mungu Hanibariki, na kuniacha bila faraja ndani yangu, kana kwamba moto mkuu unachoma ndani yangu, na hakuna amani au

furaha, na hata ingawa adabu na nidhamu ya Mungu kamwe iko na mimi, katika adabu ya Mungu na hukumu ninao uwezo wa kuona tabia Yake ya haki. Mimi hupata furaha katika hili; hakuna kitu cha thamani zaidi au cha maana zaidi ya hili katika maisha. Ingawa ulinzi Wake na huduma vimekuwa adabu kali, hukumu, laana na mipigo, bado mimi hupata starehe katika mambo haya, kwani yanaweza kunitakasa bora zaidi na kunibadilisha, yanaweza kunileta karibu na Mungu zaidi, yanaweza kufanya niweze kumpenda Mungu zaidi, na yanaweza kufanya upendo wangu kwa Mungu uwe safi zaidi. Hii inanifanya niwe na uwezo wa kutimiza wajibu wangu kama kiumbe, na inanichukua mbele za Mungu na kuniweka mbali na ushawishi wa Shetani, ili nisije tena nikamtumikia Shetani. Wakati siishi chini ya himaya ya Shetani, na ninaweza kutoa kila kitu nilicho nacho na kile ninachoweza kwa ajili ya Mungu, bila kubakisha chochote—hapo ndipo nitakuwa nimeridhika kikamilifu. Ni adabu ya Mungu na hukumu Yake ndiyo iliyoniokoa, na maisha yangu hayawezi kutengwa kutoka kwenye adabu na hukumu ya Mungu. Maisha yangu hapa duniani yamo chini ya himaya ya Shetani, na isingekuwa huduma na ulinzi na adabu ya Mungu na hukumu Yake, ningeliishi daima chini ya himaya ya Shetani, na, zaidi ya hayo, singekuwa na nafasi au njia ya kuishi kwa kudhihirisha maisha yenye maana. Ni wakati tu ambapo adabu ya Mungu na hukumu kamwe hainiachi, ndio nitakapokuwa na uwezo wa kutakaswa na Mungu. Ni kwa maneno makali na tabia ya haki ya Mungu, na hukumu kuu ya Mungu, ndipo nimepata ulinzi mkuu, na kuishi katika mwanga, na kupokea baraka za Mungu. Kuwa na uwezo wa kutakaswa, na kujiweka huru kutokana na Shetani, na kuishi chini ya utawala wa Mungu—hii ndiyo baraka kubwa zaidi katika maisha yangu leo.” Huu ndio ulimwengu wa juu zaidi aliopitia Petro.

Hizi ndizo hali ambazo mwanadamu lazima afikie baada ya kufanywa mkamilifu. Kama huwezi kufikia kiasi hiki, basi huwezi kuishi kwa kudhihirisha maisha yenye maana. Mwanadamu anaishi katika mwili, ambayo ina maana anaishi katika kuzimu ya binadamu, na bila hukumu na adabu ya Mungu, mwanadamu ni mchafu kama Shetani. Mwanadamu atawezaje kuwa mtakatifu? Petro aliamini kwamba adabu na hukumu ya Mungu ndio uliokuwa ulinzi bora zaidi wa mwanadamu na neema kubwa. Ni kwa njia ya adabu na hukumu ya Mungu ndipo mwanadamu angeweza kugutuka, na kuchukia mwili, na kumchukia Shetani. Nidhamu kali ya Mungu inamweka huru kutokana na ushawishi wa Shetani, inamweka huru kutokana na dunia yake ndogo, na inamruhusu kuishi katika mwanga wa uwepo wa Mungu. Hakuna wokovu bora zaidi kuliko adabu na hukumu! Petro aliomba, “Ee Mungu! Mradi tu Wewe unaniadibu na kunihukumu, nitajua kwamba Wewe hujaniacha. Hata kama Huwezi kunipa furaha au amani, na kufanya niishi katika mateso, na kunirudi mara nyingi, bora tu Hutaniacha moyo wangu utakuwa na amani. Leo hii, adabu Yako na hukumu umekuwa ulinzi wangu bora na baraka yangu kubwa. Neema unayonipa inanilinda. Neema unayoweka juu yangu leo ni kielelezo cha tabia Yako ya

haki, na ni adabu na hukumu; zaidi ya hayo, ni majaribu, na, zaidi ya hapo, ni maisha ya mateso.” Petro alikuwa na uwezo wa kuweka kando raha ya mwili na kutafuta mapenzi zaidi na ulinzi zaidi, kwa sababu alikuwa amepata neema nyingi kutoka kwa adabu na hukumu ya Mungu. Katika maisha yake, kama mwanadamu anatamani kutakaswa na kufikia mabadiliko katika tabia yake, kama anatamani kuishi kwa kudhihirisha maisha yenye maana, na kutimiza wajibu wake kama kiumbe, basi lazima akubali adabu na hukumu ya Mungu, na lazima asiruhusu nidhamu ya Mungu na kipigo cha Mungu kiondoke kwake, ili aweze kujiweka huru kutokana na kutawalwa na ushawishi wa Shetani na kuishi katika mwanga wa Mungu. Ujue kwamba adabu ya Mungu na hukumu ni mwanga, na mwanga wa wokovu wa mwanadamu, na kwamba hakuna baraka bora zaidi, neema au ulinzi bora kwa ajili ya mwanadamu. Mwanadamu anaishi chini ya ushawishi wa Shetani, na yupo katika mwili; kama yeye hatatakaswa na kupokea ulinzi wa Mungu, basi mwanadamu atakuwa milele mpotovu zaidi. Kama yeye anataka kumpenda Mungu, basi lazima atakaswe na kuokolewa. Petro aliomba, “Mungu, wakati Unanitendea wema ninapata furaha, na kuhisi faraja; wakati unaniadibu, najisikia faraja kubwa zaidi na furaha. Ingawa mimi ni mdhaifu, na kuvumilia mateso yasiyotajika, ingawa kuna machozi na huzuni, Unajua kwamba huzuni huu ni kwa sababu ya kutotii kwangu, na kwa sababu ya udhaifu wangu. Mimi ninalia kwa sababu siwezi kukidhi hamu Yako, nahisi huzuni na majuto kwa sababu mimi sitoshi kwa mahitaji Yako, lakini niko tayari kufikia ulimwengu huu, niko tayari kufanya yote niwezayo ili nikuridhishe. Adabu Yako imeniletea ulinzi, na kunipa wokovu bora; hukumu Yako inazidi ustahimili Wako na uvumilivu Wako. Bila adabu Yako na hukumu, singefurahia huruma Yako na rehema. Leo, naona zaidi kwamba upendo wako umepita mipaka ya mbinguni na kuwa bora ya yote. Upendo wako sio tu huruma na fadhili; hata zaidi ya hayo, ni adabu na hukumu. Adabu Yako na hukumu imenipa mengi. Bila adabu Yako na hukumu, hakuna hata mmoja angetakaswa, na hakuna hata mmoja angeweza kupata upendo wa Muumba. Ingawa nimevumilia mamia ya majaribio na mateso, na hata nimekuwa karibu na kifo, haya yameniruhusu kukujua Wewe kwa kweli na kupata wokovu mkuu. Kama adabu Yako, hukumu na nidhamu vingondoka kutoka kwangu, basi ningeishi gizani, chini ya himaya ya Shetani. Mwili wa binadamu una faida gani? Kama adabu Yako na hukumu ingeniwacha, ingekuwa kana kwamba Roho Wako alikuwa ameniacha, ni kama Wewe Haukuwa tena pamoja nami. Kama ingekuwa vile, ni jinsi gani ningeendelea kuishi? Kama Wewe utanipa ugonjwa, na kuchukua uhuru wangu, naweza kuendelea kuishi, lakini adabu Yako na hukumu vikiondoka kutoka kwangu, sitakuwa na njia ya kuendelea kuishi. Kama ningeikuwa bila adabu Yako na hukumu, ningepoteza upendo Wako, upendo ambao ni mkuu sana mpaka sina maneno ya kuueleza. Bila Upendo wako, ningeishi chini ya miliki ya Shetani, na singeweza kuuona uso wako mtukufu. Ningewezaje kuendelea kuishi? Giza kama hili, maisha kama haya, singeweza kuvumilia. Mimi kuwa na wewe ni kama kukuona Wewe, hivyo ni jinsi gani ningeweza

kukuacha? Ninakusihi, nakuomba usichukue faraja yangu kubwa kutoka kwangu, hata kama ni maneno machache tu ya uhakikisho. Nimefurahia upendo wako, na leo hii siwezi kuwa mbali na Wewe; ningewezaje kutokupenda Wewe? Nimemwaga machozi mengi ya huzuni kwa sababu ya upendo Wako, ilhali daima nimehisi kuwa maisha kama haya ni ya maana zaidi, yenye uwezo mwingi wa kuniimarisha, yenye uwezo zaidi wa kunibadilisha, na yenye uwezo zaidi wa kunifanya nifikie ukweli ambao lazima viumbe wawe nao.”

Maisha yote ya mwanadamu yamekuwa chini ya himaya ya Shetani, na hakuna mtu yeyote anayeweza kujitoa kutoka katika ushawishi wa Shetani yeye mwenyewe. Wote wanaishi katika dunia chafu, kwa upotovu na utupu, bila maana yoyote au thamani; wanaishi maisha ya kutojali kwa ajili ya mwili, tamaa, na kwa ajili ya Shetani. Hakuna maana yoyote kwa kuwepo kwao. Mwanadamu hana uwezo wa kupata ukweli utakaomweka huru kutoka kwa ushawishi wa Shetani. Ingawa mwanadamu anaamini katika Mungu na anasoma Biblia haelewi jinsi ya kujitoa kutoka kwa ushawishi wa Shetani. Kutoka kitambo, watu wachache sana wametambua siri hii, wachache sana wameielewa. Hivyo, hata kama mwanadamu anamchukia Shetani, na anachukia mwili, hajui jinsi ya kujitoa kutoka kwa ushawishi mkuu wa Shetani. Je, leo bado hamjamilikiwa na Shetani? Hamjuti juu ya matendo yenu ya uasi, zaidi ya hayo, hamhisi kama wachafu na waasi. Baada ya kumpinga Mungu, bado mna amani ya moyo na mnahisi utulivu mwingi. Je, utulivu wako si kwa sababu wewe ni mpotovu? Je, hii amani ya mawazo haitokani na kuasi kwako? Mwanadamu anaishi katika jehanamu ya binadamu, anaishi katika ushawishi wa giza la Shetani; mkabala katika ardhi, mapepo yanaishi na mwanadamu, yakienea katika mwili wa mwanadamu. Duniani, hauishi katika Paradiso ya kupendeza. Mahali ambapo ulipo ni ulimwengu wa Shetani, jehanamu ya binadamu, dunia ya chini. Mwanadamu asipotakaswa, basi yeye ni wa uchafu; asipolindwa na kutunzwa na Mungu, basi yeye bado ni mfungwa wa Shetani; asipohukumiwa na kuadibiwa, basi hatakuwa na njia ya kuepuka ukandamizaji na ushawishi mbaya wa Shetani. Tabia potovu unayoonyesha, na tabia ya uasi unayoishi kwa kudhihirisha inatosha kuonyesha kwamba bado unaishi katika himaya ya Shetani. Kama akili na mawazo yako hayajatakaswa, na tabia yako haijahukumiwa na kuadibiwa, basi nafsi yako yote bado inadhibitiwa na himaya ya Shetani, akili yako bado inadhibitiwa na Shetani, mawazo yako yanatawaliwa na Shetani, na nafsi yako yote inadhibitiwa na mikono ya Shetani. Je, unajua uko umbali gani, sasa, na viwango alivyokuwa navyo Petro? Je, wewe unamiliki kiwango hicho? Ni kiasi gani unajua kuhusu adabu na hukumu ya wakati wa leo? Unacho kiasi gani cha yale Petro alipata kujua? Iwapo, leo, huna uwezo wa kutambua, je utaweza kupata maarifa haya baadaye? Mtu mzembe na mwoga kama wewe hawezi kujua kuhusu adhabu na hukumu. Ukifuata amani ya kimwili, na raha za kimwili, basi hutakuwa na njia yoyote ya kutakaswa, na mwishowe utarudishwa kwa Shetani, kwa sababu hali unayoishi kwa kudhihirisha ni ya Shetani, na ya

mwili. Vitu vilivyo sasa, watu wengi hawayafuati maisha, kwa hivyo inamaanisha kuwa hawajali kuhusu kutakaswa, ama kuingia katika uzoefu wa ndani ya maisha. Je, watawezaje kufanywa kuwa wakamilifu? Wale wasiofuata maisha hawana fursa ya kufanywa wakamilifu, na wale wasiofuata maarifa ya Mungu, na hawafuati mabadiliko katika tabia zao, hawataweza kuepuka ushawishi wa giza wa Shetani. Kwa kuashiria maarifa yao kuhusu Mungu na kuingia kwao katika mabadiliko ya tabia zao, hawana umakini kuzihusu, kama wale wanaoamini katika dini pekee, na wale wanaofuata tu sherehe na kuhudhuria huduma za kawaida. Je, hiyo si kupoteza wakati? Kama, kwa imani yake kwa Mungu, mwanadamu hayuko makini katika mambo ya maisha, hafuati kuingia katika ukweli, hazingatii mabadiliko katika tabia yake, ama kufuata maarifa ya kazi ya Mungu, basi hawezi kufanywa mkamilifu. Kama unatamani kufanywa mkamilifu, lazima uelewe kazi ya Mungu. Hasa, lazima uelewe umuhimu wa adabu na hukumu Yake, na kwa nini kazi hii inafanywa juu ya mwanadamu. Je, unaweza kukubali? Wakati wa adabu ya aina hii, unaweza kupata uzoefu na maarifa kama Petro? Ukifuata maarifa ya Mungu na ya kazi ya Roho Mtakatifu, na kuzingatia mabadiliko katika tabia yako, basi una fursa ya kufanywa mkamilifu.

Kwa wale ambao wanatakiwa kufanywa wakamilifu, hatua hii ya kazi ya kushinda ni ya lazima; Ni baada ya kushindwa tu ndipo mwanadamu anaweza kuiona kazi ya kufanywa mkamilifu. Hakuna maana kubwa ya kufanya kazi ya kushindwa, ambayo itakufanya usiwe mwenye kufaa kufanya kazi yoyote ya Mungu. Hutakuwa na uwezo wowote wa kufanya kazi yako ya kueneza injili, kwa sababu hufuati maisha, na hujibadilishi na kujifanya mpya, na hivyo basi huna uzoefu kamili wa maisha. Katika kazi hii ya hatua kwa hatua, uliwahi kuwa na nafasi ya mtendaji-huduma, na foili^[a], lakini kwa hakika usipofuata kuwa kama Petro, na ufuasi wako sio kama wenye njia ambayo Petro alifanywa mkamilifu, basi, kiasili hutapata mabadiliko katika tabia yako. Kama wewe ni mtu anayefuata kuwa mkamilifu, basi utakuwa na ushuhuda, na utasema: “Katika hii kazi ya hatua kwa hatua ya Mungu, nimekubali kazi ya Mungu ya adabu na hukumu, na hata kama nimepitia mateso mengi, nimepata kujua jinsi Mungu hufanya mwanadamu kuwa mkamilifu, nimepata kazi iliyofanywa na Mungu, nimekuwa na maarifa ya haki ya Mungu, na adabu Yake imeniokoa. Tabia Yake ya haki imekuja juu yangu, na ikaniletea baraka na neema; ni hukumu Yake na adabu ambazo zimenilinda na kunitakasa. Kama singeadibiwa na kuhukumiwa na Mungu, na kama maneno makali ya Mungu hayangekuja juu yangu, singalimjua Mungu, ama kuokolewa. Leo, naona, kama kiumbe, kwamba mtu hafurahii tu vitu vilivyoyumbwa na Muumba, lakini pia, la maana sana ni kwamba viumbe vyote watafurahia haki ya tabia ya Mungu, na kufurahia hukumu Yake ya haki, kwa sababu tabia ya Mungu ina umuhimu katika furaha ya Mwanadamu. Kama kiumbe ambaye amepotoshwa na Shetani, kila mmoja anafaa kufurahia tabia ya haki ya Mungu. Katika tabia Yake ya haki, kuna adabu na hukumu, na pia,

kuna upendo mkuu. Ingawa sina uwezo wa kupata kwa kikamilifu upendo wote wa Mungu leo, nimekuwa na bahati nzuri ya kuuona, na katika haya, nimebarikiwa.” Hii ndio njia ambayo wale waliofanywa wakamilifu hutembea na maarifa wanayoongelea. Watu hao wanafanana na Petro; wanao uzoefu sawa na wa Petro. Watu kama hao pia ndio wale ambao wamepokea maisha, na walio na ukweli. Wanapokuwa na uzoefu mpaka mwisho kabisa, wakati wa hukumu ya Mungu kwa hakika wataweza kikamilifu kujitoa katika ushawishi wa Shetani, na atakuwa wa Mungu.

Baada ya kushindwa, watu hawana ushuhuda wa kusikia. Kwa hakika wameaibisha tu Shetani, lakini hawajaishi kwa kudhihirisha ukweli wa neno la Mungu. Haujapata wokovu wa pili; umepata tu sadaka ya dhambi, ilhali haujafanywa mkamilifu—hii ni hasara kubwa. Lazima muelewe yale mnafaa kuingia ndani yake, na yale mnafaa kuishi kwa kudhihirisha, na lazima muingie ndani mwao. Kama mwishowe, hautafaulu kufanywa mkamilifu, basi hautakuwa binadamu wa kweli, na utajawa na majuto. Adamu na Hawa waliumbwa na Mungu hapo mwanzo wakiwa watu watakatifu, ni kama kusema, katika bustani ya Edeni, walikuwa watakatifu, wasiokuwa na uchafu. Walikuwa watiifu kwa Yehova, na hawakujua chochote kuhusu kuasi Yehova. Hii ni kwa sababu hawakuwa na kusumbuliwa na ushawishi wa Shetani, hawakuwa na sumu ya Shetani, na walikuwa watu wasafi kati ya binadamu wote. Waliishi katika bustani ya Edeni, bila kutiwa najisi na uchafu wowote, bila kuingiliwa na mwili, na heshima kwa Yehova. Baadaye, walipojaribiwa na Shetani, wakawa na sumu ya nyoka, na tamaa ya kuasi Yehova, na wakaishi chini ya ushawishi wa Shetani. Hapo mwanzo, walikuwa watakatifu na wenye kuheshimu sana Yehova; hivyo tu ndivyo walikuwa binadamu. Baadaye, baada ya kujaribiwa na Shetani, wakala tunda la maarifa ya kujua mazuri na mabaya, na wakaishi chini ya ushawishi wa Shetani. Waliendelea kupotoshwa na Shetani, na wakapoteza sura asili ya mwanadamu. Hapo mwanzo, mwanadamu alikuwa na pumzi ya Yehova, na hakuwa muasi hata kidogo, na hakuwa na uovu wowote katika moyo wake. Wakati huo, mwanadamu alikuwa binadamu wa kweli. Baada ya kupotoshwa na Shetani, mwanadamu akawa mnyama. Fikra zake zikajawa na uovu na uchafu, bila mazuri ama utakatifu. Je, huyu si Shetani? Umepata kujua mengi kuhusu kazi ya Mungu, ilhali haujabadilika wala kutakaswa. Bado unaishi katika himaya ya Shetani, na bado hujajitoa na kunyenyekea kwa Mungu. Huyu ni mtu ambaye ameshindwa lakini hajafanywa mkamilifu. Na mbona inasemekana kuwa mtu kama huyu hajafanywa mkamilifu? Kwa sababu mtu huyu hafuati maisha ama maarifa ya kazi ya Mungu, na hutamani tu raha za kimwili na starehe ya muda mfupi. Na kwa hivyo hakuna mabadiliko katika tabia zao, na hawajapata sura asili ya mwanadamu ilivyoumbwa na Mungu. Watu hao ni maiti zinazotembea, ni waliokufa na hawana roho! Wale wasiofuata maarifa ya mambo katika Roho, wasiofuata utakatifu, na wasiofuata kuishi kulingana na maisha ya ukweli, wanaotosheka na kushindwa kwa upande wa kanusho, na wasioweza kuishi kwa kufuata maneno ya Mungu na

kuwa binadamu watakatifu—hawa ni watu ambao hawajaokolewa. Kwani, kama hana ukweli, mwanadamu hataweza kusimama imara katika majaribu ya Mungu; wale watakaoweza kusimama imara katika majaribu ya Mungu pekee ndio wale ambao wameokolewa. Ninalotaka Mimi ni watu kama Petro, watu wanaofuata kufanywa wakamilifu. Ukweli wa leo unatolewa kwa wale ambao wanautamani na kuutafuta. Wokovu huu unapewa wale ambao wanatamani kuokolewa na Mungu, na haujakusudiwa kuwafaidi tu, lakini ili pia ili mpatwe na Mungu. Mnampata Mungu ili Mungu pia awapate. Leo nimenena hayo maneno kwenu, na mmeyasikia, na mnafaa kutenda kulingana na maneno haya. Mwishowe, mkiweka maneno haya katika matendo ndipo nitakapowapata nyinyi kupitia katika maneno haya; na pia, mtakuwa mmepata maneno haya, kumaanisha, mtakuwa mmepata wokovu mkuu. Punde mtakapofanywa wasafi, mtakuwa wanadamu halisi. Kama huwezi kuishi kulingana na ukweli, ama kuishi kulingana na aliyefanywa mkamilifu, basi inaweza kusemwa kuwa wewe si binadamu, ila wewe ni mfu anayetembea, mnyama, kwa sababu huna ukweli, ni kusema huna pumzi ya Yehova, na basi wewe ni mtu aliyekufa ambaye hana roho! Ingawa unaweza kuwa na ushuhuda baada ya kushindwa, unachopata ni wokovu kidogo, na hujakuwa kiumbe chenye roho. Ingawa umepata adabu na hukumu, tabia yako haijafanywa upya ama kubadilishwa kama matokeo; umebaki tu ulivyokuwa, bado wewe ni wa Shetani, na wewe si mtu aliyetakaswa. Wale tu waliofanywa wakamilifu ndio wenye thamani, na watu tu kama hao ndio wamepata maisha ya kweli. Siku moja, mtu atakuambia, “Umeishuhudia kazi ya Mungu, basi zungumzia kidogo jinsi kazi Yake ilivyo. Daudi aliishuhudia kazi ya Mungu, na kuona kazi ya Yehova, Musa pia alishuhudia matendo ya Yehova, na wawili hao waliweza kuelezea juu ya matendo ya Yehova, na wangeweza kuongelea maajabu ya Yehova. Mmeona kazi iliyofanywa na Mungu mwenye mwili siku za mwisho; unaweza kuongea kuhusu hekima Yake? Unaweza kuongelea maajabu ya kazi Yake? Ni nini Mungu alihitaji kutoka kwenu, na mliyaona vipi? Mmeiona kazi ya Mungu katika siku za mwisho; maono yenu makuu ni yapi? Mnaweza kuzungumza kuhusu haya? Mnaweza kuongea juu ya tabia ya haki ya Mungu?” Utajibu nini utakapokabiliana na maswali hayo? Ukisema, “Mungu ni mwenye haki sana, Anaadibu na kutuhukumu, na kutuonyesha kwa wazi. Tabia ya Mungu kwa hakika haistahimili makosa ya mwanadamu. Baada ya kuiona kazi ya Mungu, nimejua unyama wetu, na kwa hakika nimeona tabia ya haki ya Mungu,” halafu yule mtu mwingine ataendelea kukuuliza, “Ni nini kingine unachojua kumhusu Mungu? Mtu anaingiaje katika uzima? Je, una matarajio yoyote ya kibinafsi?” Utajibu, “Baada ya kupotoshwa na Shetani, viumbe wa Mungu walikuwa wanyama, na hawakuwa na tofauti na punda. Leo, ninaishi katika mikono ya Mungu, kwa hivyo lazima nikidhi matakwa na matamania ya Muumba, na kutii kile Anachofunza. Sina chaguo lingine.” Kama unaongea kwa ujumla kama huo pekee, mtu yule hataelewa kile unachokisema. Wakikuuliza ni maarifa gani unayo juu ya kazi ya Mungu, wanazungumzia kazi uliyofanya na mambo uliyopitia binafsi. Wanataka kujua

juu ya ufahamu ulionao juu ya adabu na hukumu ya Mungu baada ya kuipitia, na kwa hiyo wanaongelea kuhusu matukio yako ya binafsi, na kuuliza uongeele ufahamu wako juu ya ukweli. Kama huwezi kuongelea mambo haya, hii inadhihirisha kwamba hujui lolote kuhusu kazi ya leo. Wewe huzungumza kuhusu maneno ya kupotosha, au yale yanayojulikana na kila mtu; hujapitia matukio yoyote halisi, wala huna dutu katika maarifa yako, na huna ushuhuda wa ukweli, na hivyo wengine hawatashawishiwa na mambo yako. Usiwe mfuasi tu wa kumtazama Mungu, na usifuate kile kinachokufanya utake kuchunguza. Kwa kutokuwa moto ama baridi utajiangamiza na kuchelewesha maisha yako. Lazima ujitoe kutoka kwa utazamaji na kutofanya chochote na uwe wa kufuata vitu vyema na kuushinda udhaifu wako, ili uweze kupata ukweli na kuishi kwa kudhihirisha maisha ya ukweli. Hakuna kitu cha kuogopesha kuhusu udhaifu wako, na kasoro zako sio shida yako kubwa. Shida yako kubwa, na kasoro yako kubwa, ni kutokuwa baridi ama moto na kutokuwa na hamu ya kuutafuta ukweli. Shida kubwa na nyinyi wote ni hali ya uoga ambapo mnaridhika na hali ilivyo, na kungoja mkitazama tu. Hiki ndicho kizuizi chenu kikuu, na adui mkubwa kwa harakati yenu ya kutafuta ukweli. Kama unatii tu kwa sababu maneno Ninayosema ni makubwa, basi huna maarifa kwa kweli, wala huuthamini ukweli. Kutii kama kwako si ushuhuda, na Siukubali utiifu wa aina hii. Mtu anaweza kukuuliza, “Mungu wako anatoka wapi hasa? Huyu Mungu wako ana kiini gani hasa?” Utajibu, “Dutu yake ni adabu na hukumu.” Kisha anaendelea, “Je, Mungu si wa huruma na upendo kwa mwanadamu? Je, hujui hivyo?” Utasema, “Huyo ni Mungu wa wengine. Ni Mungu ambaye watu wa dini wanaamini, si Mungu wetu.” Wakati watu kama wewe wanaeneza injili, ukweli unapotoshwa na wewe, basi una maana gani? Watu wengine watawezaje kuupata ukweli kutoka kwako? Huna ukweli, na huwezi kuongea chochote cha ukweli, ama, zaidi ya hayo, huwezi kuishi kwa kudhihirisha ukweli. Ni nini kinakuhitimisha kuishi mbele ya Mungu? Unapoeneza injili kwa wengine, na unaposhiriki kuhusu ukweli, na kuwa na ushuhuda kuhusu Mungu, kama huwezi kuwatwaa kuja kwa Mungu, watayakataa maneno yako. Je, hutakuwa mpotezaji wa nafasi? Umeona mengi kuhusu kazi ya Mungu, ilhali ukiongelea ukweli, haeleweki. Je, wewe si bure tu? Wewe una maana gani? Mngewezaje kuwa mmeshuhudia kazi nyingi ya Mungu vile, ilhali hamna ufahamu kuhusu Mungu? Wakiuliza ni maarifa gani hasa uliyonayo ya Mungu, huna la kusema, au unajibu na kitu kisichoambatana na swali—ukisema kuwa Mungu ni mkuu, kuwa baraka ambayo umepokea ni uadhimisho wa Mungu, na kwamba hakuna bahati kuu kushinda kumwona Mungu kibinafsi. Kuna thamani gani ndani ya kusema hivyo? Ni maneno matupu yasiyo na maana! Kwa kuwa umeshuhudia kazi nyingi ya Mungu, je, unajua kuwa uadhimisho wa Mungu ni ukweli? Lazima ujue kazi ya Mungu, na hapo tu ndipo utakuwa na ushuhuda wa kweli kwa Mungu. Watu ambao hawajaupata ukweli watawezaje kumshuhudia Mungu?

Ikiwa kazi nyingi, na maneno mengi, hayajakuwa na mabadiliko kwako, basi wakati

utakapofika wa kueneza kazi ya Mungu hutaweza kufanya kazi yako, na utaaibika na kufedheheshwa. Wakati huo utajisikia kuwa una deni kubwa kwa Mungu, kwamba maarifa yako juu ya Mungu ni juujuu. Usipofuata maarifa ya Mungu leo, Akiwa bado Anafanya kazi, basi baadaye itakuwa umechelewa. Mwishowe hutakuwa na maarifa yoyote ya kuongelea— utawachwa tupu, bila chochote. Ni nini utakachotumia kupeana uwajibikaji wako kwa Mungu? Je, una uchungu kuangalia Mungu? Unafaa kujitahidi katika shughuli yako sasa, ili mwishowe uweze, kama, Petro, kujua jinsi adabu na hukumu ya Mungu ina manufaa kwa binadamu, na bila adabu na hukumu Yake mwanadamu hawezi kuokolewa, na atazidi kuzama kwenye ardhi chafu, ndani zaidi kwenye tope. Wanadamu wamepotoshwa na Shetani, wamefitini wenyewe kwa wenyewe, wamekuliana njama wenyewe kwa wenyewe, wamepoteza heshima yao kwa Mungu, na uasi wao ni mkubwa sana, fikira zao ni nyingi, na wote ni wa Shetani. Bila adabu na hukumu ya Mungu, tabia potovu ya mwanadamu haiwezi kutakaswa na hangeweza kuokolewa. Kinachoelezwa na Mungu anayefanya kazi katika mwili hasa ndicho kile kinachoelezwa na Roho, na kazi afanyayo inafanyika kulingana na ile ifanywayo na Roho. Leo, kama huna maarifa yoyote juu ya hii kazi, basi wewe ni mpumbavu sana, na umepoteza mengi! Kama hujapata wokovu wa Mungu, basi imani yako ni ya kidini, na wewe ni Mkristo wa dini. Kwa sababu umeshikilia mafundisho yaliyokufa, umepoteza kazi mpya ya Roho Mtakatifu; wengine, wanaofuata upendo wa Mungu, wanaweza kupata ukweli na uhai, ambapo imani yako haiwezi kupata idhini ya Mungu. Badala yake, umekuwa mtenda maovu, mtu afanyaye vitendo vyenye kuharibu na vya chuki, umekuwa kilele cha utani wa Shetani, na mfungwa wa Shetani. Mungu si wa kuaminiwa na mwanadamu, lakini wa kupendwa na yeye, na kufuatwa na kuabudiwa na yeye. Usipomfuata leo, basi siku itakuja ambapo utasema, “Hapo zamani mbona sikumfuata Mungu vizuri sikumridhisha vizuri, sikufuatilia mabadiliko katika tabia yangu ya maisha? Najuta kutojiwasilisha kwa Mungu kwa wakati ufao, na kutotafuta maarifa ya neno la Mungu. Mungu alisema mengi wakati ule; nilikosa vipi kufuata? Nilikuwa mjinga!” Utajichukia mpaka kiwango fulani. Leo, huamini maneno ninayosema, na huyatili maanani; wakati utakapofika kwa hii kazi kuenezwa, na unaona ukamilifu wake, utajuta, na wakati huo utakuwa bubu. Kuna baraka, ilhali hujui kuzifurahia, na kuna ukweli, ilhali hujui kuufuata. Je, hujiletei dharau? Leo ingawa hatua inayofuata kwa kazi ya Mungu haijaanza, hakuna kitu cha kipekee juu ya mahitaji yanayohitajika kwako na unachoulizwa kuishi kwa kudhihirisha. Kuna kazi nyingi, na ukweli mwingi; Je, hazina maana kujulikana na wewe? Je, adabu na hukumu ya Mungu haitoshi kuamsha roho yako? Je, adabu na hukumu ya Mungu haitoshi kukufanya ujichukie? Umetosheka kuishi katika ushawishi wa Shetani, kwa amani na furaha, na raha kidogo ya kimwili? Je, wewe si mtu wa chini zaidi kati ya watu wote? Hakuna aliye mpumbavu kuliko wale ambao wameona wokovu lakini hawaufuati ili kuupata; hawa ni watu ambao wanalafua mwili na kufurahia Shetani. Unatumai kwamba imani yako kwa Mungu haitakuwa na changamoto ama dhiki, ama mateso

yoyote. Unafuata vile vitu ambavyo havina maana, na huambatanishi faida yoyote kwa maisha, badala yake kuweka mawazo ya fujo kabla ya ukweli. Huna maana! Unaishi kama nguruwe—kuna tofauti gani kati yako, nguruwe na mbwa? Je, hao wasiofuata ukweli na badala yake wanafuata mapenzi ya kimwili, si wote ni wanyama? Hao waliokufa na bila roho si wafu wanaotembea? Maneno mangapi yamenenwa kati yenu? Je, kazi kidogo imefanywa kati yenu? Ni kiasi gani nimetoa kati yenu? Na mbona hujapata chochote? Una nini cha kulalamikia? Je, si ni kweli kuwa hujapata chochote kwa sababu unapenda mwili sana? Na ni kwa sababu mawazo yako ni ya fujo sana? Je, si kwa sababu wewe ni mpumbavu sana? Kama huna uwezo wa kupata baraka hizi, unaweza kumlaumu Mungu kwa kutokukuokoa? Unachofuata ni cha kukuwezesha kupata amani baada ya kumwamini Mungu—watoto wako wawe huru kutokana na magonjwa, ili mme wako apate kazi nzuri, ili mwana wako apate mke mwema, binti wako apate mme anayeheshimika, ili ndume na farasi wako walime shamba vizuri, kwa mwaka wa hali ya anga nzuri kwa mimea yako. Hili ndilo unalolitafuta. Harakati yako ni kuishi kwa starehe, ili ajali isipate familia yako, ili upepo ukupite, ili uso wako usiguswe na changarawe, ili mazao ya familia yako yasipate mafuriko, ili usiguswe na majanga yoyote, kuishi katika mikono ya Mungu, kuishi kwenye kiota chenye joto. Mwoga kama wewe, anafuata mwili kila wakati—je, una moyo, una roho? Si wewe ni mnyama? Nakupa njia ya ukweli bila kukuuliza chochote, ilhali hauifuati. Je, wewe ni wale wamwaminio Mungu? Nahifadhi uhai wa ukweli wa binadamu juu yako, ila hauufuati. Je, una tofauti kati ya nguruwe na mbwa? Nguruwe hawafuati maisha ya binadamu, hawafuati kutakaswa, na hawaelewi maana ya maisha. Kila siku wanapokula na kushiba, wanalala. Nimekupa njia ya ukweli, ila hujaipata: Wewe u mkono mtupu. Je, unakubali kuendelea na maisha haya, maisha ya nguruwe? Umuhimu wa watu hao kuwa hai ni nini? Maisha yako ni ya kudharauliwa na kutoheshimika, unaishi huku ukiwa na uchafu na uzinzi, na hufuati lengo lolote; je, si maisha yako ni ya kutoheshimika kwa yote? Je, una ujasiri wa kumtazamia Mungu? Ukiendelea kuwa na uzoefu wa haya, je, si utakosa kupata chochote? Umepewa njia ya ukweli, lakini kama utaipata ama hapana inategemea na kutafuta kwako. Watu husema Mungu ni Mungu wa haki, na kwamba mradi tu mwanadamu atamfuata mpaka mwisho, basi Hatakuwa na upendeleo kwa mwanadamu, kwani Yeye ni mwenye haki. Je, mwanadamu akimfuata mpaka mwisho kabisa, Mungu anaweza kumtupa mwanadamu nje? Sina upendeleo kwa mwanadamu yeyote, na Huwahukumu wanadamu wote kwa tabia Yangu ya haki, ilhali kuna mahitaji yanayofaa Ninayohitaji kutoka kwa mwanadamu, na Ninahitaji yakamilishwe na wanadamu wote, bila kujali ni nani. Sijali kiwango cha kufuzu kwako au kuheshimiwa kwako; najali tu kama utatembea kwa njia Yangu, na kama unapenda na una kiu ya ukweli. Kama huna ukweli, na unaleta aibu katika jina Langu, na matendo yako ni kinyume cha njia Yangu, kufuata tu bila kujali, basi wakati huo nitakupiga na kukuadhibu kwa uovu wako, na utakuwa na nini la kusema? Utaweza kusema Mungu si mwenye haki? Leo kama umezingatia maneno ambayo

nimenena, basi wewe ni mtu ambaye Namkubali. Unasema umeumia ukifuata Mungu, kwamba umemfuata kwa marefu na mapana, na umeshiriki na yeye katika wakati mzuri na mbaya, lakini hujaishi kulingana na maneno yaliyosemwa na Mungu; unataka tu kukimbia huku na kule kwa ajili ya Mungu na kujitumia kwa ajili ya Mungu kila siku, na hujafikiria kuishi kwa kudhihirisha maisha yenye maana. Unasema pia, “Kwa vyovyote, naamini Mungu ni mwenye haki. Nimeteseka kwa ajili Yake, nikashughulika kwa ajili Yake, kujitoa kikamilifu Kwake, na nimefanya bidii ingawa sijapata kutambuliwa; Yeye hakika atanikumbuka.” Ni ukweli kwamba Mungu ni mwenye haki, na haki hii haijatiwa doa na uchafu wowote: Haina mapenzi ya binadamu, na haijatiwa doa na mwili, ama kitendo chochote cha binadamu. Wale wote ambao ni waasi na wako kwa upinzani, na hawazingatii njia Zake wataadhibiwa; hakuna atakayesamehewa, na hakuna atakayeepuka! Watu wengine husema, “Leo nakimbia juu yako; mwisho ukifika, utanipa baraka kidogo?” Sasa Nakuuliza, “Umezingatia maneno Yangu?” Haki unayoongelea inategemea matendo. Unafikiria kwamba Mimi ni mwenye haki, na asiye na mapendeleo kwa binadamu wote, na kwamba wale wanifuatao hadi mwisho wataokolewa na kupata baraka Yangu. Kuna maana ya ndani kwa maneno Yangu kwamba “wale wote wanifuatao hadi mwisho wataokolewa”: Wale wanifuatao mpaka mwisho ndio Nitakaowapata, ni wale, baada ya kushindwa Nami, watautafuta ukweli na kufanywa wakamilifu. Ni hali gani umepata? Umepata kunifuata hadi mwisho, lakini nini kingine? Je, umezingatia maneno Yangu? Umekamilisha moja kati ya tano ya mahitaji Yangu, ilhali huna mpango wa kumaliza manne yaliyobaki. Umepata ile njia rahisi, na ukafuata ukifikiria umebahatika. Kwa mtu kama wewe, haki Yangu ni adabu na hukumu, ni adhabu ya haki, na ni adhabu ya haki kwa watenda maovu wote; wale wote wasiotembea kwa njia Yangu wataadhibiwa, hata kama watafuata mpaka mwisho. Hii ndio haki ya Mungu. Wakati tabia hii ya haki inapodhihirishwa katika adhabu ya mwanadamu, mwanadamu atakosa la kusema, na kujuta kwamba, alipokuwa akimfuata Mungu hakutembea katika njia Yake. “Wakati huo niliteseka kidogo tu nikimfuata Mungu, lakini sikutembea katika njia ya Mungu. Kuna udhuru gani? Hakuna namna ila kuadibiwa!” Ila kwa akili yake anafikiria, “Nimefuata hadi mwisho, hata Ukiniadibu haitakuwa adabu kali, na baada ya kuadibu kwa kuchosha, bado Utanihitaji. Najua Wewe ni mwenye haki, na Hutanifanyia hivyo milele. Mimi si kama wale watakaofagiliwa nje; wale watakaofagiliwa watapokea adabu kuu, na adabu Yangu itakuwa kidogo.” Adabu ya Mungu ya tabia ya haki si unavyosema. Sio kwamba wale ambao wanatubu dhambi zao kila wakati wataadibiwa kwa huruma. Haki ni utakatifu, na ni tabia ambayo haivumilii makosa ya mwanadamu, na yale yote ambayo ni machafu na hayajabadilika ndiyo shabaha ya chukizo kwa Mungu. Haki ya Mungu si sheria, lakini amri ya utawala: Ni amri ya utawala katika ufalme, na hii amri ya utawala ni adhabu ya haki kwa yeyote asiye na ukweli na hajabadilika, na hakuna kiwango cha wokovu. Mwanadamu akiwekwa kulingana na aina, wazuri watazawadiwa na wabaya kuadhibiwa. Ndio wakati hatima

ya mwanadamu itawekwa wazi, na ndio ni wakati ambao kazi ya wokovu itafika mwisho, baada ya hapo, kazi ya kuokoa binadamu haitafanyika tena, na adabu italetwa kwa wale waliotenda maovu. Watu wengine husema, “Mungu hukumbuka kila mmoja ambaye huwa kando Yake kila wakati. Hatasahau hata mmoja wetu. Tumehakikishiwa kufanywa wakamilifu na Mungu. Hatawakumbuka wowote walio chini, wale kati yao watakaofanywa wakamilifu wana uhakika kuwa watakuwa duni kutuliko sisi, tunaokutana na Mungu kila wakati; kati yetu hakuna ambaye amesahaulika na Mungu, wote tumeshakubaliwa na Mungu, na tunalo hakikisho la kufanywa wakamilifu na Mungu.” Nyote mna mawazo ya aina hii. Je, hii ni haki? Je, umeweka ukweli katika vitendo au la? Kwa hakika unaeneza uvumi kama huu—huna aibu!

Leo, watu wengine wanatafuta kutumiwa na Mungu, lakini baada ya kushindwa hawawezi kutumika moja kwa moja. Kwa maneno yaliyonenwa leo, kama, wakati Mungu anapotumia watu, bado huwezi kuyakamilisha, basi hujafanywa mkamilifu. Kwa maneno mengine, kufika kwa mwisho wa wakati ambao mwanadamu anafanywa mkamilifu kutabaini iwapo mwanadamu atatupwa ama atatumiwa na Mungu. Wale walioshindwa ni mifano wa kutojijhusisha na uhasi tu; ni sampuli na mifano, lakini si chochote ila ni ujazio wa wimbo. Ni wakati tabia ya maisha ya mwanadamu imebadilika, na amepata mabadiliko ndani na nje, ndipo atakapokuwa amefanywa mkamilifu. Leo, ni nini utakacho, kushindwa ama kufanywa mkamilifu? Ni nini unachotamani kupata? Umetimiza masharti ya kufanywa mkamilifu? Ni yapi ambayo bado unakosa? Unapaswa kujihami vipi, na utaweka mikakati ipi ili kuondoa upungufu wako? Utaingia vipi katika njia ya kufanywa mkamilifu? Utajiwasilisha vipi kikamilifu? Unataka kufanywa mkamilifu, je, unafuata utakatifu? Je, wewe ni mtu anayetaka kupitia hukumu na kuadibu ili uweze kutakaswa? Unatafuta kutakaswa, kwa hivyo una nia ya kukubali adabu na hukumu? Unataka kujua Mungu, lakini je, una maarifa ya adabu na hukumu Yake? Leo, kazi nyingi Anayofanya kwenu ni adabu na hukumu; ufahamu wako wa kazi hii ni upi, ambayo imetekelezwa juu yako? Je, adabu na hukumu ambayo umepitia imekutakasa? Imekubadilisha? Imekuwa na mabadiliko yoyote kwako? Umechoka sana na kazi hii nyingi ya leo—laana, hukumu na ufichuzi—ama unaona mambo haya yakiwa ya manufaa kwako? Unapenda Mungu, lakini kwa nini unampenda Yeye? Je, unampenda Mungu kwa sababu umepokea neema kidogo? Ama unapenda Mungu baada ya kupata amani na furaha? Ama unampenda Mungu baada ya kutakaswa na adabu na hukumu yake? Ni nini hasa kinachokufanya umpende Mungu? Ni masharti yapi ndiyo Petro alikamilisha ili afanywe mkamilifu? Baada ya kufanywa mkamilifu, ni njia gani muhimu ndiyo ilitumiwa kudhihirisha? Je, alimpenda Bwana Yesu kwa sababu alitamani kuwa na Yeye, ama kwa sababu hangeweza kumuona, ama ni kwa sababu alikuwa ameshutumiwa? Ama alimpenda Bwana Yesu zaidi kwa sababu alikubali mateso ya shida, na alikuwa amejua uchafu wake na kuasi, alikuwa amepata kujua utakatifu wa Bwana? Je, mapenzi yake kwa Mungu yalikuwa safi kwa sababu ya

adabu na hukumu ya Mungu, ama kwa sababu ya kitu kingine? Ni nini hasa? Unampenda Mungu kwa sababu ya neema ya Mungu, na kwa sababu leo amekupa baraka kidogo. Je, huu ni upendo wa ukweli? Unapaswa kumpenda Mungu vipi? Je, unapaswa kukubali kuadibu na hukumu Yake, na, baada ya kuona tabia Yake yenye haki, uweze kumpenda kwa kweli, hivi kwamba umeshawishika kabisa, na kuwa na maarifa Yake? Kama Petro, unaweza kusema kwamba huwezi kumpenda Mungu vya kutosha? Je, unachofuata kishindwe baada ya adabu na hukumu, ama kutakaswa, kimelindwa na kushughulikiwa baada ya adabu na hukumu? Ni gani kati ya haya unayofuata? Je, maisha yako yana maana ama hayana maana wala dhamani? Unataka mwili ama ukweli? Unataka hukumu, ama faraja? Baada ya kupitia na kuiona kazi nyingi ya Mungu, na baada ya kuuona utakatifu na haki ya Mungu, unafaa kumfuata vipi? Unapaswa kutembea vipi katika njia hii? Utahitajika kuweka mapenzi ya Mungu katika matendo kivipi? Je, adabu na hukumu ya Mungu zimekuwa na athari yoyote kwako? Kama una maarifa ya adabu na hukumu ya Mungu itategemea jinsi unavyoishi kwa kudhihirisha, na kiwango gani unapenda Mungu! Kinywa chako kinasema unampenda Mungu, ilhali unachoishi kwa kudhihirisha ni tabia nzee, zilizo potovu; humchi Mungu, na sembuse kuwa na dhamiri. Je, watu wa aina hii wanampenda Mungu? Je, watu wa aina hii ni waaminifu kwa Mungu? Je, wao ni wale wanaokubali adabu na hukumu ya Mungu? Unasema unampenda na kumwamini Mungu, ilhali huachi hisia zako. Katika kazi yako, kuingia kwako, maneno uzungumzayo, na katika maisha yako, hakuna udhihirisho wa mapenzi yako kwa Mungu, na hakuna heshima kwa Mungu. Je, huyu ni mtu ambaye amepata adabu na hukumu? Mtu kama huyu anaweza kuwa Petro? Wale walio kama Petro wana maarifa, lakini je, wanaishi kulingana nayo? Leo, ni hali gani inahitaji mwanadamu aishi kwa kudhihirisha maisha ya ukweli? Maombi ya Petro hayakuwa maneno matupu yaliyotoka mdomoni mwake? Hayakuwa maneno kutoka moyoni mwake? Petro aliomba tu, na hakuweka ukweli katika matendo? Kufuata kwako ni kwa niaba ya nani? Utajiwezesha kupokea ulinzi na utakaso wakati wa hukumu na kuadibu kwa Mungu? Je, adabu na hukumu ya Mungu haina faida yoyote kwa mwanadamu? Je, hukumu yote ni adhabu? Je, amani na furaha, baraka ya vitu vya dunia na faraja, ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu? Mwanadamu akiishi katika mazingira mazuri ya raha, bila maisha ya hukumu, anaweza kutakaswa? Iwapo mwanadamu anataka kubadilika na kutakaswa, anafaa kukubali vipi kufanywa mkamilifu? Ni njia gani unayopaswa kuchagua leo?

Tanbihi:

a. “Foili” inahusu mtu au kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Ni Lazima Muielewe Kazi—Msifuate kwa Rabsha!

Kwa sasa kuna watu wengi ambao huamini kwa njia ya rabsha. Udadisi wenu ni mkubwa mno,

tamaa yenu ya kufuatilia baraka ni kubwa mno, na hamu yenu ya kufuatilia maisha ni ndogo mno. Waumini katika Yesu siku hizi wamejaa shauku. Yesu atawakaribisha katika nyumba ya mbinguni—je, wao hawawezi kuamini? Watu wengine ni waumini katika maisha yao yote, wameamini kwa miaka arobaini au hamsini, na hawachoki kamwe kusoma Biblia. Hii ni kwa sababu wanafikiri^[a] kwamba bila kujali kinachotokea, mradi wao wanaamini, wataingia mbinguni. Mmemfuata Mungu kwa njia hii kwa miaka michache tu, lakini tayari mnajitahidi sana na hamna uvumilivu tena. Hii ni kwa sababu hamu yenu ya kupata baraka ina nguvu mno. Nyinyi kuitembea njia hii ya kweli kunadhibitiwa na hamu yenu ya kupata baraka na nyoyo zenu chunguzi. Hamna ufahamu mwingi wa hatua hii ya kazi. Mengi ya yale Ninayoyasema leo siyo kuongea kwa wale watu wanaoamini katika Yesu; hayaongewi hata kidogo kurudisha pigo dhidi ya dhana zao. Kwa kweli, hizi dhana zinazofichuliwa ni dhana zile zile ambazo zipo kati yenu, kwa sababu hamuelewi ni kwa nini Biblia imewekwa chini, kwa nini Ninasema kuwa kazi ya Yehova imezeeka, na kwa nini Ninasema kuwa kazi ya Yesu imezeeka. Kwa kweli, mna dhana nyingi ambazo hamjazipa sauti. Mna dhana nyingi ambazo zimefungiwa ndani ya mioyo yenu, na nyinyi mnafuata umati tu. Je, mnadhani kuwa dhana zenu ni chache? Ni kwamba tu kuwa hamzitungumzii, na hakuna cha ziada! Kwa kweli, mnafuata tu kwa uzembe, hamtafuti njia ya kweli kamwe, na kwa makusudi hamji kupata uzima. Mna mtazamo wa kutaka tu kuona kitakachotokea. Kwa sababu hamjaziacha dhana zenu za zamani, hakuna yeyote kati yenu ambaye ameweza kujitoa mwenyewe kikamilifu. Baada ya kufika wakati huu, bado mnaendelea kuwa na wasiwasi kuhusu majaliwa yenu wenyewe, fikira zenu zikipinduka mchana na usiku, msiweze kuyaachiilia. Je, unafikiri kuwa Mafarisayo ambao Mimi nawaongelea ni “wazee” katika dini? Je, si nyinyi ni wawakilishi wa Mafarisayo wa kuendelea mbele zaidi wa enzi ya sasa? Je, unafikiri kwamba wale watu Ninaowataja wanaoniangalia Mimi kwa makini dhidi ya Biblia wanarejelea tu wale wataalamu wa Biblia wa nyanja za kidini? Je, unadhani kwamba Ninapozungumza juu ya wale ambao kwa mara nyingine wanamtundika Mungu msalabani Nazungumzia viongozi wa jamii za kidini? Je, si nyinyi ni wahusika bora kabisa ambao mnaigiza wajibu huu? Je, unafikiri kwamba katika maneno yote Ninayoyanena kurudisha pigo dhidi ya dhana za watu ni mzaha kwa wachungaji na wazee wa dini? Si nyinyi pia mmeshiriki katika mambo haya yote? Je, mnafikiri kuwa mna dhana chache tu? Ni kwamba tu nyote mmejifunza kuwa mahiri sana sasa. Hamzungumzii mambo ambayo hamyafahamu ama kusaliti hisia zenu kuyahusu, lakini mioyo yenu ya heshima na mioyo yenu ya utii haipo tu. Kama mnavyoona, kusoma, kuzingatia, na kusubiri ni matendo yenu makuu ya leo. Mmejifunza kuwa mahiri mno. Je! mnajua, hata hivyo, kwamba hii ni aina yenu ya saikolojia ya ujanja? Je, mnafikiri kuwa wakati wa mahiri kwa upande wenu utawasaidia kuepuka kuadibiwa kwa milele? Mmejifunza kuwa wenye “busara” mno! Na baadhi ya watu huniuliza Mimi mambo kama: “Siku moja, wakati watu wa kidini huniuliza, nini, ‘Mbona Mungu wako hajatenda muujiza hata mmoja?’

Ninafaa kuelezea vipi?” Sasa, siyo tu kwamba watu wa dini watauliza mambo kama hayo. Badala yake, ni kwamba huielewi kazi ya leo, na una dhana nyingi mno. Je, bado hujui ni nani Ninayemrejelea Ninapotaja maafisa wa kidini? Unajua Ninawaelezea nani Biblia? Je, hujui ni kwa nani Ninazungumzia wakati Ninapoeleza kwa mifano hatua tatu za kazi? Je, Singesema vitu hivi, mngeridhishwa kwa urahisi hivyo? Je, mngenyenyekea kwa urahisi hivyo? Je, ni rahisi kwenu kushusha hizo dhana za zamani? Hasa wale “watu halisi” ambao hawajawahi kumtii yeyote—je, wangeweza kutii kwa urahisi sana? Najua kwamba ingawa mna daraja ya chini ya ubinadamu, mna ubora duni sana wa tabia, mna akili ambazo hazijakua sana, na hamna historia ndefu za kumwamini Mungu, kwa kweli mna dhana nyingi kabisa, na asili yenu ya kawaida ni ya kutomnyenyekea yeyote kwa wepesi. Leo, hata hivyo, mnaweza kunyenyekea kwa sababu mnalazimishwa na hamjiwezi; Ninyi ni chui-milia katika kizimba cha chuma, bila uwezo wa kutumia ujuzi wenu. Ingekuwa vigumu kuruka hata kama mngekuwa na mabawa. Ingawa hamjapewa baraka, mnataka kufuata unyonyo. Hata hivyo, hii si roho yenu ya “mtu mzuri”, ila ni kwamba mmeangushwa kabisa, na mnataka kuchanganyikiwa. Ni kwamba kazi yote hii imewaangusha kabisa. Ikiwa kungekuwa na chochote ambacho mngeweza kufikia, hamngekuwa watiifu kama mliyovyo leo, kwa sababu awali, nyote mlikuwa punda mwitu nyikani. Hivyo kinachosemwa leo hakielekezwi tu kwa watu wa dini na madhehebu mbalimbali, na siyo kurudisha pigo dhidi ya dhana zao; badala yake ni kurudisha pigo dhidi ya dhana zenu.

Hukumu ya haki imeanza. Je, Mungu bado atatumikia kama sadaka ya dhambi kwa watu? Je, Mungu atachukua nafasi ya daktari mkuu kwa watu tena? Je, Mungu hana mamlaka zaidi ya hivi? Kundi la watu tayari limefanywa kamilifu, na tayari wamenyakuliwa mbele ya kiti cha enzi. Je, Yeye bado atawafukuza pepo na kuwaponya wagonjwa? Si hili ni jambo la kale? Je, ushuhuda utawezekana kwa kwendelea jinsi hii? Mungu ametundikwa msalabani mara moja, hivyo Atasulubishwa milele? Baada ya kuwafukuza pepo mara moja, Atawafukuza milele? Je, si hili ni sawa na udhalilishaji? Ni wakati tu hatua hii ya kazi inapokuwa juu zaidi kuliko ile ya awali ndipo enzi husonga mbele. Kisha siku za mwisho zitafikiwa, na wakati utakuja ambapo enzi itahitimishwa. Watu wanaofuatilia ukweli kwa hiyo wanapaswa kuzingatia kuwa dhahiri juu ya maono. Huu ndio msingi. Kila wakati Ninapofanya ushirika nanyi kuhusu maono, daima Mimi huona vigubiko vya jicho vya baadhi ya watu vikinyong’onyea na wakianza kushikwa na usingizi, bila kutaka kusikiliza. Wengine huuliza: “Ni kwa nini wewe husikilizi?” Yeye husema, “Hili halisaidii maisha yangu au kuingia kwangu katika hali halisi. Tunachotaka ni njia za matendo.” Wakati Mimi siongei juu ya njia za matendo, na Ninaongea juu ya kazi, anasema, “Punde unapoongea juu ya kazi mimi huanza kushikwa na usingizi.” Sasa Ninaanza kuzungumza juu ya njia za matendo, na anaanza kuchukua muhtasari. Ninaanza tena kuzungumza juu ya kazi hiyo, na anarejelea kutosikiliza. Je, mnajua ni nini mnachopaswa kujiandaa nacho? Jambo moja

ni maono juu ya kazi, na jambo jingine ni matendo yako. Lazima ufahamu mambo yote mawili. Kama huna maono katika jitihada zako za kufanya maendeleo katika maisha, basi huna msingi. Kama una njia za matendo tu na huna maono hata kidogo, na huna ufahamu wowote wa kazi ya mpango mzima wa usimamizi, basi wewe ni bure. Lazima uelewe ukweli wa kipengele cha njozi, na kwa ukweli kuhusu matendo, unahitaji kupata njia mwafaka za kutenda mara unapozelewa; unahitaji kutenda kulingana na maneno, na uingie kulingana na hali zako. Maono ndiyo msingi, na usipozingatia hili, hutaweza kufuata hadi mwisho. Unapopitia njia hii, ama utapotea au kuanguka chini na kushindwa. Hakutakuwa na njia ya kufanikiwa! Watu ambao hawana maono makubwa kama msingi wao wanaweza tu kushindwa na si kufanikiwa. Huwezi kusimama imara! Je, unajua kuamini katika Mungu ni nini? Je, unajua kumfuata Mungu ni nini? Bila maono, ni njia gani ungeitembea? Katika kazi ya leo, kama huna maono hutaweza kufanywa mkamilifu kamwe. Unaamini katika nani? Kwa nini unamwamini Yeye? Mbona unamfuata Yeye? Je, unaamini kama aina ya mchezo? Je, unashughulikia maisha yako kama aina ya mtu anayechezewa? Mungu wa leo ndiye maono makubwa zaidi. Je, ni kiasi gani Chake unachokijua? Je, ni kiasi gani Chake ambacho umekiona? Je, baada ya kumwona Mungu wa leo, msingi wa imani yako katika Mungu u salama? Je, unafikiri kwamba mradi unafuata katika njia hii iliyovurugika, utapata wokovu? Unafikiri unaweza kuvua samaki katika maji yenye tope? Je, ni rahisi hivyo? Je, ni maoni mangapi yako kuhusu kile ambacho Mungu wa leo anasema umeweka chini? Je, una maono ya Mungu wa leo? Ufahamu wako wa Mungu wa leo umesimamia wapi? Daima wewe huamini kuwa unaweza kumpata Yeye^[b] kwa kumfuata tu, kwamba kwa kumuona Yeye, na kwamba hakuna yeyote anayeweza kukukwepa. Usifikiri kwamba kumfuata Mungu ni rahisi sana. Cha muhimu ni kwamba ni lazima umjue Yeye, lazima uijue kazi Yake, na lazima uwe na nia ya kuvumilia shida kwa ajili Yake, uwe na nia ya kutoa maisha yako kwa ajili Yake, na uwe na nia ya kukamilishwa na Yeye. Haya ndiyo maono ambayo unapaswa kuwa nayo. Haitafaidi kama wewe daima unafikiria kufurahia neema. Usifikiri kwamba Mungu yupo tu kwa ajili ya starehe za watu, na kukirimu neema kwa watu. Wewe ulifikiri vibaya! Kama mtu hawezi kuhatarisha maisha yake ili kufuata, ama mtu hawezi kuacha kila mali ya dunia ili kufuata, basi kwa uhalisi hataweza kufuata hadi mwisho. Lazima uwe na maono kama msingi wako. Kama siku ya kupatwa kwako na maafa itakapokuja, unapaswa kufanya nini? Bado ungeweza kufuata? Usiseme kwa wepesi kama utaweza kufuata hadi mwisho. Ni bora kwanza ufungue macho yako wazi kabisa ili uone wakati wa sasa ni upi. Ingawa sasa mnaweza kuwa kama nguzo za hekalu, wakati utakuja ambapo nguzo hizi zote zitatafunwa na funza, na kusababisha hekalu kuanguka, kwa sababu kwa sasa kuna maono mengi sana ambayo mmelesa. Mnachozingatia tu ni dunia zenu wenyewe ndogo, na hamjui njia iliyo ya kutegemewa kabisa, njia iliyo mwafaka zaidi ya kutafuta ni ipi. Hamtilii maanani maono ya kazi ya leo, na hamyashikilii mambo haya mioyoni mwenu. Je, mmefikiria kwamba siku moja

Mungu atawaweka katika mahali pasipojulikana? Je, mnaweza kuwazia siku ambayo huenda Nikawapokonya kila kitu, ni kipi kingewakumba? Nguvu yenu siku hiyo ingekuwa vile ilivyo sasa? Je, imani yenu ingejitokeza tena? Katika kumfuata Mungu, lazima myajue maono haya makubwa ambayo ni “Mungu.” Hili ndilo suala muhimu zaidi. Pia, msidhani kwamba katika kuachana na watu wa kidunia ili kuwa watakatifu kwamba nyinyi ni familia ya Mungu. Leo ni Mungu Mwenyewe ambaye anafanya kazi miongoni mwa uumbaji. Ni Mungu aliyekuja miongoni mwa watu kufanya kazi Yake mwenyewe, si kutekeleza kampeni. Miongoni mwenu, hakuna hata wachache ambao wanaweza kujua kwamba kazi ya leo ni kazi ya Mungu aliye mbinguni ambaye amekuwa mwili. Siyo juu ya nyinyi kufanywa watu waliojipambanua wenye vipaji. Badala yake, ni kuwasaidia kujua umuhimu wa maisha ya binadamu, kujua hatima ya binadamu, na kuwasaidia kumjua Mungu na uzima Wake. Unapaswa kujua kwamba wewe ni uumbaji mikononi mwa Muumba. Unachopaswa kufahamu, unachopaswa kufanya, na unavyopaswa kumfuata Mungu—je, huu si ni ukweli unaopaswa kuuelewa? Je, haya si ni maono ambayo unapaswa kuyaona?

Wakati ambapo mtu ana maono ana msingi. Unapotenda kwa msingi wa kanuni hii, itakuwa rahisi zaidi kuingia ndani. Kwa njia hii hutakuwa na wasiwasi punde unapopata msingi wa kuingia ndani, na itakuwa rahisi sana kwako kuingia ndani. Kipengele hiki cha kuyaelewa maono, cha kuielewa kazi ya Mungu ni muhimu. Lazima muwe mmejiandaa na kipengele hiki. Kama hujajiandaa na kipengele hiki cha ukweli, na wewe huongea tu juu ya njia za matendo, hii ni kasoro kubwa. Nimegundua kwamba wengi wenu hamsisitizi kipengele hiki, na wakati unaposikiliza kipengele hiki cha ukweli ni kama tu kusikiliza maneno ya mafundisho. Siku moja huenda ukapoteza. Kuna baadhi ya maneno sasa ambayo huyafahamu na huyakubali; kwa hiyo unapaswa kutafuta kwa uvumilivu, na siku itakuja utakapoelewa. Jiandae kidogo kidogo. Hata kama unaelewa mafundisho machache tu ya kiroho, ni bora kuliko kutoyazingatia. Ni bora kuliko kutoelewa mafundisho yoyote kamwe. Haya yote ni ya kusaidia kwa kuingia kwako, na yataondoa mashaka hayo yako. Ni bora kuliko kujazwa kwako na dhana. Ni bora zaidi kuwa na maono haya kama msingi. Bila kuwa na wasiwasi kamwe, inawezekana kuingia ndani kwa mikogo na majivuno. Kwa nini kujisumbua daima ukifuata kwa kukanganyikiwa kwa njia ya shaka? Je, hiyo si ni kama kuziba masikio yako wakati unaiba kengele? Ni jambo zuri kama nini kuingia katika ufalme kwa mikogo na majivuno! Kwa nini ujawe wasiwasi? Je, si huku hasa kungekuwa ni kupitia mateso? Unapokuwa na ufahamu wa kazi ya Yehova, wa kazi ya Yesu, na wa hatua hii ya kazi, basi utakuwa na msingi. Sasa unaweza kufikiri kwamba ni rahisi sana. Baadhi ya watu husema, “Wakati unapofika na Roho Mtakatifu anaanza kazi hii kubwa, nitaweza kuzungumza kuhusu mambo haya yote. Ukweli kwamba kwa kweli sielewi sasa ni kwa sababu Roho Mtakatifu hajanipatia nuru sana.” Si rahisi sana; sio kwamba huko tayari kuikubali

ukweli^[e] sasa, na kisha wakati utakapowadia utaitumia kwa ustadi. Si lazima iwe hivyo! Unaamini kuwa sasa umejiandaa vizuri sana, na kwamba haingekuwa shida kuwajibu wale watu wa kidini na wanadhaharia wakuu zaidi, na hata kuwakanusha. Je, ungeweza kweli kufanya hivyo? Je, ni ufahamu upi unaoweza kuuzungumzia na huo uzoefu wako duni tu? Kuwa umejiandaa na ukweli, kupigana vita ya ukweli, na kutoa ushuhuda kwa jina la Mungu si kile unachofikiri ndicho—kwamba mradi Mungu yuko kazini yote yatakamilishwa. Wakati huo labda utatatizwa na swali fulani, na utafadhaishwa. Cha muhimu ni kama uko dhahiri kuhusu hatua hii ya kazi au la, na ni kiasi gani unaielewa. Ikiwa huwezi kuyashinda majeshi ya adui, na wala kuyashinda majeshi ya kidini, basi si wewe ungekuwa bure? Kama umepata uzoefu wa kazi ya leo, ukaiona kwa macho yako mwenyewe na kuisikia kwa masikio yako mwenyewe, lakini mwishowe unashindwa kushuhudia, bado unathubutu kuendelea kuishi? Ungeweza kukabiliana na nani? Usifikiri kwa kawaida sana sasa. Kazi baadaye haitakuwa rahisi kama unavyofikiri itakuwa. Kupigana vita vya ukweli si rahisi au kawaida sana. Sasa unahitaji kujiandaa. Usipokuwa umejiandaa kwa ukweli sasa, wakati utakapowadia na Roho Mtakatifu hafanyi kazi kwa njia ya mwujiza, basi utakuwa umechanganyikiwa.

Tanbihi:

- a. Maandishi ya awali hayana neno “wanafikiri.”
- b. Maandishi ya awali hayana neno “Yeye.”
- c. Maandishi ya wali hayana neno “ukweli.”

Jinsi Unavyopaswa Kuitembea Sehemu ya Mwisho ya Njia

Ninyi sasa mko katika kipindi cha mwisho cha njia, na ni sehemu muhimu ya njia. Labda umepitia mateso mengi, umefanya kazi nyingi, umesafiri barabara nyingi, na umesikiliza mahubiri mengi; labda haijakuwa rahisi kufika pale ulipo sasa. Ikiwa huwezi kuvumilia mateso unayokabiliwa nayo kwa sasa na ukiendelea kama ulivyofanya hapo zamani, basi huwezi kukamilishwa. Maneno haya hayajakusudiwa kukuogofya—ni ukweli. Baada ya Petro kupitia kazi nyingi ya Mungu, alipata ufahamu wa mambo fulani, na pia utambuzi mwingi. Alikuwa kuelewa mambo mengi kuhusu kanuni ya huduma, na baadaye aliweza kujitoa kikamilifu kwa yale ambayo Yesu alimwaminia. Usafishaji mkubwa ambao alipokea kwa kiasi kikubwa ulikuwa kwa sababu, kwa mambo ambayo alikuwa amefanya mwenyewe, alihisi kwamba alikuwa na deni kubwa la Mungu, na kwamba hangeweza kumlipa kamwe. Petro alitambua pia kwamba mwanadamu ni mpotovu sana, jambo ambalo lilimfanya ahisi hatia katika dhamiri yake. Yesu alikuwa amemwambia Petro mambo mengi, lakini katika wakati ambapo mambo haya yalisemwa, aliweza kuwa na ufahamu mdogo tu, na wakati mwingine bado alikuwa na upinzani na uasi kiasi. Baada ya Yesu kusulubiwa msalabani, mwishowe alipitia mwamko fulani, na ndani

mwake alihisi maumivu makali ya kujilaumu mwenyewe. Mwishowe, ilifikia hatua ambapo alihisi haikukubalika kuwa na maoni yoyote ambayo hayakuwa sahihi. Alijua hali yake mwenyewe vizuri sana, na pia alijua utakatifu wa Bwana vizuri sana. Kwa sababu hiyo, moyo wa kumpenda Bwana ulikua ndani yake hata zaidi, na akazingatia zaidi maisha yake mwenyewe. Kwa sababu ya hili alipitia shida nyingi, na ingawa wakati mwingine ilikuwa kama kwamba alikuwa na ugonjwa hatari na hata ilionekana kama kwamba alikuwa amekufa, baada ya kusafishwa kwa njia hii mara nyingi, alijielewa zaidi, na akawa na upendo wa kweli kwa Bwana. Inaweza kusemekana kuwa maisha yake yote yalitumika katika usafishaji, na hata zaidi ya hayo, katika kuadibu. Uzoefu wake ulikuwa tofauti na wa mtu mwingine yeyote, na upendo wake ulizidi ule wa mtu yeyote ambaye hajakamilishwa. Sababu ya kuchaguliwa kwake kama mfano ni kwa sababu alipitia uchungu mwingi kabisa katika maisha yake, na yale aliyoyapitia yalifanikiwa zaidi. Kama mnaweza kweli kuitembea sehemu ya mwisho ya njia kama vile Petro alivyofanya, basi hakuna kiumbe yeyote anayeweza kuwanyang'anya baraka zenu.

Petro alikuwa mtu mwenye dhamiri, lakini hata akiwa na ubinadamu aliokuwa nao, bila kuzuilika, alikuwa na maoni mengi ya upinzani na ya uasi katika wakati huo alipoanza kumfuata Yesu kwa mara ya kwanza. Lakini alipokuwa akimfuata Yesu, hakuchukulia mambo haya kwa uzito, akiamini kuwa hivi ndivyo watu walipaswa kuwa. Kwa hivyo, mwanzoni hakuhihi lawama yoyote na wala hakushughulikiwa. Yesu hakuchukulia majibu ya Petro kwa uzito, wala Hakuyatilia maanani, bali Aliendelea tu na kazi ambayo Alipaswa kufanya. Hakuwahi kutafuta makosa madogo madogo kwa Petro na wengine. Unaweza kusema: “Inawezekana kwamba Yesu hakujua kuhusu maoni haya waliyokuwa nayo?” La hasha! Ni kwa sababu alimwelewa Petro vyema—kwa kweli, inaweza kusemwa kwamba Alikuwa na ufahamu wa juu kuhusu—ndiyo maana Yesu hakuchukua hatua yoyote dhidi yake. Aliwachukia wanadamu lakini pia Aliwahurumia. Je, si kuna watu wengi miongoni mwenu sasa ambao ni wapinzani kama tu alivyokuwa Paulo, na walio na maoni mengi kama vile Petro alivyokuwa nayo kwa Bwana Yesu wakati huo? Nakwambia, itakuwa bora usipoamini sana katika hisi yako ya tatu, hisi yako ya mtazamo, ambayo siyo ya kutegemewa na iliyoharibiwa kabisa na upotoshaji wa Shetani zamani. Je, unafikiri kwamba mtazamo wako ni kamili na hauna dosari? Paulo alimpinga Bwana Yesu mara nyingi, lakini Yesu hakujibu. Inawezekana kwamba Yesu aliweza kuponya wagonjwa na kufukuza pepo, lakini hakuweza kumfukuza yule “pepo” aliyekuwa ndani ya Paulo? Ni kwa nini ni kwamba huku Paulo akiendelea kuwakamata wanafunzi wa Yesu kwa ukaidi, ni baada tu ya Yesu kufufuka na kupaa kwenda mbinguni ndipo mwishowe Yesu alimwonekana akiwa njiani kwenda Dameski na kumpiga chini? Inawezekana kwamba Bwana Yesu alijibu polepole sana? Au ni kwa sababu Hakuwa na mamlaka yoyote wakati Alikuwa katika mwili? Je, unafikiri kuwa wakati wewe ni mharibifu kwa siri na mpinzani wakati ambapo Sioni ya kwamba Sijui kuhusu

hilo? Je, unafikiri kwamba mabaki ya nuru unayopata kutoka kwa Roho Mtakatifu yanaweza kutumiwa kunipinga Mimi? Wakati Petro hakuwa mkomavu, alikuwa na maoni mengi kumhusu Yesu, kwa hivyo mbona hakulaumiwa? Hivi sasa, watu wengi wanafanya mambo bila lawama, na hata wanapoambiwa wazi kuwa kile wanachofanya si sahihi, bado hawasikilizi. Je, hilo si kwa sababu ya uasi wa mwanadamu kabisa? Nimesema mengi sana sasa, lakini bado huna hata chembe ya mtazamo wa dhamiri, kwa hivyo utawezaje kuitembea sehemu ya mwisho ya njia, kuendelea kutembea hadi njia itakapomalizika? Je, huhisi kuwa hili ni swali lenye uzito mkubwa?

Baada ya watu kushindwa, wanaweza kutii mipango ya Mungu; wana imani yao na ridhaa yao ambayo kwayo wanampenda Mungu, na wanategemea vitu hivi kumfuata. Kwa hivyo sehemu ya mwisho ya njia inaweza kutembewaje? Katika siku zako za kupitia mateso, lazima uvumilie shida zote, na lazima uwe radhi kuteseka; ni kwa njia hii tu ndiyo unaweza kuitembea sehemu hii ya njia vizuri. Je, unafikiri ni rahisi sana kuitembea sehemu hii ya njia? Unapaswa kujua ni kazi gani unayopaswa kutimiza; lazima mwongeze ubora wenu wa tabia na mjiandae na ukweli wa kutosha. Hii siyo kazi ya siku moja au mbili, na siyo rahisi kama vile unavyofikiri! Kuitembea sehemu ya mwisho ya njia kunategemea imani na ridhaa uliyo nayo kweli. Pengine huwezi kumwona Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani yako, au pengine huwezi kugundua kazi ya Roho Mtakatifu kanisani, kwa hivyo wewe huna rajua na unasikitika na kukata tamaa sana kwa siku za usoni. Hususani, mashujaa wakuu wa zamani wote wameanguka—je, yote haya si pigo kwako? Je, unapaswa kuyaonaje mambo haya? Je, una imani, au huna? Unaelewa kazi ya leo kikamilifu, au huielewi? Vitu hivi vinaweza kuamua ikiwa unaweza kuitembea sehemu ya mwisho ya njia kwa mafanikio.

Ni kwa nini inasemekana kwamba sasa mko kwenye sehemu ya mwisho ya njia? Ni kwa sababu mmeelewa kila kitu mnachopaswa kuelewa, na ni kwa sababu Nimewaambia kila kitu ambacho watu wanapaswa kutimiza. Pia, Nimewaambia kuhusu kila kitu ambacho mmeaminiwa nacho. Kwa hivyo, kile mnachokitembea sasa ni sehemu ya mwisho ya njia ambayo kwayo Ninawaongoza watu. Nahitaji tu kwamba mpate uwezo wa kuishi kwa kujitegemea; wewe utakuwa na njia ya kufuata daima na kila wakati, utaongeza ubora wako wa tabia kama zamani, utasoma maneno ya Mungu kwa kawaida, na kuishi maisha ya kawaida ya binadamu. Sasa Ninakuongoza uishi hivi, lakini katika siku za usoni wakati Sikuongozi, bado utaweza kuishi hivi? Je, utaweza kuendelea? Hili ndilo alilopitia Petro: Wakati Yesu alikuwa akimwongoza, hakuwa na ufahamu; alikuwa asiyejali kama mtoto, na hakuyachukulia mambo aliyofanya kwa uzito. Ilikuwa tu baada ya Yesu kuondoka ndipo alianza maisha yake ya binadamu wa kawaida. Maisha yake yenye maana yalianza tu baada ya Yesu kuondoka. Hata ingawa alikuwa na akili fulani ya ubinadamu wa kawaida na mambo fulani ambayo mtu wa kawaida anapaswa kuwa

nayo, hata hivyo yale aliyopitia na ufuatiliaji wake wa kweli havikuwa na mwanzo mpya hadi Yesu alipoondoka. Je, hali yenu ya sasa ni ipi? Sasa, Mimi ninakuongoza hivi, na wewe unafikiri hili ni jambo zuri sana. Hakuna mazingira na majaribu yanayokukumba, lakini kwa njia hii hakuna njia ya kuona wewe kweli una kimo cha aina gani, wala hakuna njia yoyote ya kuona kama wewe kweli ni mtu anayefuatilia ukweli. Unasema kwa mdomo wako kwamba unaelewa kiini chako mwenyewe, lakini haya ni maneno matupu. Ni katika siku za usoni tu, ukweli utakapokujia, ndipo ufahamu wako utathibitishwa. Sasa, wewe una ufahamu wa aina hii: “Ninaelewa kwamba mwili wangu umepotoka sana, na kiini cha miili ya watu ni kuasi na kumpinga Mungu. Kuweza kupokea hukumu na kuadibu kwa Mungu ndiyo njia ambayo Yeye huwainua watu. Nimeelewa hilo sasa, na niko tayari kulipa upendo wa Mungu.” Lakini hili ni rahisi kusema. Baadaye wakati dhiki, majaribu, na mateso yatakukumba, haitakuwa rahisi kupitia vitu hivi. Mtafuata hivi kila siku, lakini bado hamwezi kuendelea kupitia matukio yenu. Itakuwa mbaya zaidi ikiwa Nitawaacha na Niwapuuze kabisa; watu wengi wataanguka chini na kugeuka kuwa nguzo ya chumvi, alama ya aibu. Matokeo kama hayo yanawezekana kuwepo sana. Je, huogopi au kuwa wasiwasi kuhusu hili? Petro alipitia mazingira ya aina hiyo na alipitia mateso ya aina hiyo, lakini bado alisimama imara. Ukipitishwa katika mazingira hayo, je, utaweza kusimama imara? Vitu ambavyo Yesu alisema na kazi ambayo Alifanya alipokuwa duniani vilimpa Petro msingi, na ilikuwa kwa msingi huu ndiyo aliitembea njia yake ya baadaye. Je, mnaweza kufikia kiwango hicho? Njia ambazo umetembea na ukweli ambao umeelewa—je, vinaweza kuwa msingi wako ambao kwao unaweza kusimama imara katika siku zijazo? Je, vitu hivi vinaweza kuwa maono yako ya kusimama imara baadaye? Nitawaambia ukweli—mtu anaweza kusema kwamba yale ambayo watu wanaelewa sasa yote ni mafundisho. Hii ni kwa sababu hawana uzoefu wa vitu vyote ambavyo wanaelewa. Kwamba umeweza kuendelea hadi sasa ni kwa sababu umeongozwa na mwanga mpya kikamilifu. Si kwa sababu kimo chako kimefikia kiwango fulani, lakini badala yake ni kwa sababu maneno Yangu yamekuongoza hadi siku ya leo; si kwa sababu wewe una imani kubwa, bali ni kwa sababu ya hekima ya maneno Yangu, ambayo yalikufanya usiweze kufanya chochote ila kufuata wakati huo wote hadi leo. Nisingeweza kunena sasa, Nisingeweza kutamka sauti Yangu, usingeweza kuendelea na ungeacha kusonga mbele mara moja. Je, hiki si kimo chenu halisi? Hamjui mnapaswa kuingia kutoka katika vipengele vipi na mnapaswa kufidia mnachokosa kutoka katika vipengele vipi. Hamwelewi jinsi ya kuishi kwa kudhihirisha maisha ya binadamu yenye maana, jinsi ya kulipa upendo wa Mungu, au jinsi ya kushuhudia kwa njia yenye nguvu na kubwa. Hamwezi kabisa kufanikisha mambo haya. Ninyi ni wavivu na ni wapumbavu! Kile mnachoweza kufanya ni kuegemea kitu kingine tu, na kile mnachoegemea ni mwanga mpya na Yule aliye mbele, Akiwaongoza. Kwamba umeweza kuendelea kuishi hadi leo ni kwa sababu umeutegemea mwanga mpya kabisa na matamshi ya hivi karibuni kabisa. Ninyi hamko kabisa kama Petro

ambaye alikuwa hodari wa kufuatilia njia ya kweli, au kama Ayubu, ambaye aliweza kumwabudu Yehova kwa kujitoa kikamilifu na kuamini kwamba Yehova alikuwa Mungu bila kujali jinsi Yehova alivyomjaribu, na ikiwa Alimbariki au la. Je, wewe una uwezo wa kufanya hilo? Je, ninyi mmeshindwaje? Kipengele kimoja ni hukumu, kuadibu, na laana, na kipengele kingine ni siri zinazowashinda. Ninyi nyote ni kama punda. Ikiwa yale Ninayozungumza kuhusu si ya juu sana vya kutosha kwenu, ikiwa hakuna siri, basi hamwezi kushindwa. Ikiwa ingekuwa ni mtu anayehubiri na kila wakati ahubiri kuhusu mambo yale yale kwa kipindi cha muda, nyote mngeondoka na kutawanyika ndani ya miaka miwili; hamngeweza kuendelea. Hamjui jinsi ya kuingia kwa kina zaidi, wala hamwelewi jinsi ya kufuatilia ukweli au njia ya uzima. Kile mnachoelewa ni kupokea kitu kinachoonekana kuwa kipya kwenu, kama vile kusikia kuhusu siri au maono, au jinsi Mungu alivyokuwa Akifanya kazi, au matukio aliyopitia Petro, au maelezo ya nyuma ya kusulubiwa kwa Yesu.... Mko tayari kusikia kuhusu mambo haya tu, na kadiri mnavyosikiliza zaidi ndivyo mnavyopata nguvu zaidi. Mnayasikiliza haya yote ili muondoe huzuni na uchovu wenu tu. Maisha yenu yanahimiliwa kikamilifu na vitu hivi vipya. Je, unafikiri kwamba umefika mahali ulipo leo kwa ajili ya imani yako mwenyewe? Je, hiki si kimo kidogo cha kusikitisha unachomiliki? Uadilifu wenu uko wapi? Ubinadamu wenu uko wapi? Je, mna uzima wa binadamu? Je, mna vipengele vingapi vinavyohitajika kwa ajili ya kukamilishwa? Je, kile Ninachosema si ukweli? Ninazungumza na kufanya kazi kwa njia hii, lakini bado mnakuwa makini kwa nadra sana. Wakati mnafuata, pia mnachunga. Kila wakati mna mwonekano wa kutojali, na kila wakati mnaongozwa kama wanyama. Hivi ndivyo ninyi nyote mmeendelea; kile kilichowaongoza hadi pale mlipo leo kimekuwa kuadibu, usafishaji, na kurudiwa. Ikiwa mahubiri fulani kuhusu kuingia katika uzima pekee yangehubiriwa, si ninyi nyote mngeponyoka zamani? Kila mmoja wenu ni mwenye kupenda makuu zaidi kuliko mwingine, lakini kwa kweli matumbo yenu yamejaa maji machafu tu! Umeweza tu kuendelea hadi sasa kwa sababu wewe umekuja kuelewa siri chache, mambo fulani ambayo wanadamu hawajawahi kuelewa hapo awali. Hamna sababu ya kutofuata, kwa hivyo mmeweza tu kujikaza na kufuata umati. Haya ni matokeo ambayo yamepatikana tu kupitia maneno Yangu, na hakika silo jambo ambalo ninyi wenyewe mmetimiza. Hamna chochote cha kujivunia. Kwa hivyo, katika hatua hii ya kazi mmeongozwa hadi siku ya leo kimsingi kupitia maneno. Vinginevyo, ni nani kati yenu ambaye angeweza kutii? Ni nani angeweza kuendelea kuwepo hadi leo? Tangu mwanzo mlitaka kuondoka fursa ya kwanza iwezekanayo itokeapo, lakini hamkuthubutu kufanya hivyo; hamkuwa na ujasiri. Hadi leo, mmekuwa mkifuata shingo upande.

Ilikuwa tu baada ya Yesu kusulubiwa msalabani na kuondoka ndiyo Petro alianza kuifuata njia yake mwenyewe na kuanza kuitembea njia aliyopaswa kuitembea; alianza kujiandaa baada tu ya kuona upungufu wake na kasoro zake. Aliona kwamba alikuwa na upendo mdogo sana kwa

Mungu na hiari yake ya kuteseka haikutosha, kwamba hakuwa na utambuzi wowote na kwamba hakuwa na akili. Aliona kwamba kulikuwa na mambo mengi ndani yake ambayo hayakulingana na mapenzi ya Yesu, na kwamba kulikuwa na mambo mengi ambayo yalikuwa ya uasi na upinzani na yaliyotiwa najisi mapenzi ya wanadamu. Ilikuwa tu baada ya hili ndiyo alipata kuingia katika kila kipengele. Yesu alipokuwa akimwongoza, Yesu aliifunua hali yake na Petro aliikubali na kukubaliana na kile ambacho Yesu alisema, lakini bado alikosa ufahamu wa kweli mpaka baadaye. Hiyo ilikuwa kwa sababu wakati huo, hakuwa na uzoefu wala maarifa ya hali yake mwenyewe. Hiyo ni kusema, kwa sasa Natumia maneno tu kuwaongoza, na haiwezekani kuwakamilisha katika kipindi kifupi na mtawekewa mipaka katika kuweza kuelewa na kujua ukweli. Hii ni kwa sababu kukushinda wewe na kukushawishi katika moyo wako ndiyo kazi ya sasa na ni baada tu ya watu kushindwa ndiyo wataweza kukamilishwa. Hivi sasa, maono hayo na ukweli huo ambao wewe unaelewa yanaweka msingi kwa ajili ya matukio utakayopitia katika siku zijazo; katika dhiki za siku zijazo nyote mtakuwa na uzoefu wa vitendo wa maneno haya. Baadaye, majaribu yatakapokujia na upitie dhiki, utakumbuka maneno unayosema leo, ambayo ni: “Haijalishi ni dhiki, majaribu au maafa yapi makubwa ninayokumbana nayo, lazima nimridhishe Mungu.” Fikiria matukio aliyopitia Petro na kisha matukio aliyopitia Ayubu—wewe utaamshwa na maneno ya leo. Ni kwa njia hii tu ndiyo imani yako inaweza kutiwa msukumo. Wakati huo, Petro alisema kwamba hakustahili kupokea hukumu na kuadibu kwa Mungu, na wakati utakapofika pia utakuwa tayari kuwafanya watu wote waone tabia ya Mungu ya haki kupitia kwako. Utakubali hukumu na kuadibu Kwake bila kusita, na hukumu, kuadibu na kulaani Kwake vitakuwa faraja kwako. Sasa, haikubaliki kabisa kwako kutojiandaa na ukweli. Bila ukweli, sio tu kwamba hutaweza kusimama imara katika siku zijazo, lakini pia huenda usiweze kuipitia kazi ya sasa. Ikiwa hii ndiyo hali, je, hutakuwa mmoja wa wale watakaotupwa nje na kuadhibiwa? Sasa hivi, hakujakuwa na ukweli wowote ambao umekujia na Nimekuruzuku katika kipengele chochote ambacho umepungukiwa; Nazungumza kutoka katika kila kipengele. Hamjapitia mateso mengi; ninyi huchukua tu kile kinachopatikana bila kulipia gharama ya aina yoyote, na, zaidi ya hayo, hamna matukio mliyopitia au utambuzi wenu halisi. Kwa hivyo, kile mnachoelewa si vimo vyenu halisi. Mmewekewa mipaka kwa ufahamu, maarifa na kuona, lakini hamjapata mavuno mengi. Ikiwa Singejali kuwahusu lakini Niwafanye mpitie matukio nyumbani kwenu wenyewe, mngekuwa mlishakimbia kurudi katika ulimwengu mkubwa wa zamani. Njia mtakayoitembea katika siku za usoni itakuwa njia ya mateso na mkiitembea kwa mafanikio njia hii ya sasa, basi mtakuwa na ushuhuda wakati ambapo mtapitia dhiki kubwa katika siku zijazo. Ikiwa unaelewa umuhimu wa maisha ya binadamu na umechukua njia inayofaas ya maisha ya mwanadamu na ikiwa katika siku za usoni utatii miundo Yake bila malalamiko yoyote au chaguo bila kujali jinsi Mungu anavyokushughulikia, na ikiwa hufanyi madai yoyote kwa Mungu, basi kwa njia hii wewe utakuwa mtu wa thamani. Sasa hivi, hujapitia dhiki, kwa hivyo unaweza kutii

chochote bila kutofautisha. Unasema kwamba vyovyote ambavyo Mungu anaongoza, hivyo ni sawa, na kwamba utatii mipango Yake yote. Mungu akuadibu au kukulaani, utakuwa tayari kumridhisha. Hata hivyo, kile unachosema sasa hakiwakilishi kimo chako hasa. Kile ambacho uko tayari kufanya sasa hakiwezi kuonyesha kuwa unaweza kufuata hadi mwisho. Dhiki kubwa zitakapokujia au utakapopitia mateso kiasi au kushurutishwa au kupitia majaribu makubwa zaidi, basi hutaweza kusema maneno hayo. Ikiwa unaweza kuwa na ufahamu wa aina hiyo wakati huo na usimame imara, hiki kitakuwa kimo chako. Je, Petro alikuwa mtu wa aina gani wakati huo? Petro alisema: “Bwana, nitayatoa maisha yangu kwa ajili Yako. Ikiwa Unataka nife, nitakufa!” Hivyo ndivyo alivyokuwa akiomba wakati huo. Alisema pia: “Hata kama wengine hawakupendi, lazima nikupende hadi mwisho. Nitakufuata kila wakati.” Hivyo ndivyo alivyosema wakati huo, lakini punde majaribu yalipomjia, alivurugika na kulia. Ninyi nyote mnajua kuwa Petro alimkana Bwana mara tatu, sivyo? Kuna watu wengi ambao watalia na kuonyesha udhaifu wa kibinadamu wakati majaribu yatakapowapata. Wewe siye bwana wako mwenyewe. Katika hili, huwezi kujidhibiti. Labda leo wewe unaendelea vizuri sana, lakini hiyo ni kwa sababu una mazingira mazuri. Hilo likibadilika kesho, wewe utaonyesha waoga na kutokuwa na uwezo kwako, kustahili dharau na kutostahili kwako. “Ujasiri” wako utakuwa tayari umetoweka, na wakati mwingine unaweza kutupa kazi yako kando na uondoke. Hii inaonyesha kuwa kile ulichoelewa wakati huo hakikuwa kimo chako halisi. Mtu lazima aangalie kimo halisi cha mtu ili aone ikiwa anampenda Mungu kweli, ikiwa ana uwezo kweli wa kutii muundo wa Mungu na ikiwa ana uwezo wa kuweka nguvu zake zote katika kutimiza kile ambacho Mungu anahitaji; na ikiwa anabaki mtiifu kwa Mungu na anampa Mungu vitu vyote vilivyo bora zaidi, hata ikimaanisha kuyatoa maisha yake mwenyewe.

Lazima ukumbuke kwamba maneno haya sasa yamenenwa: Baadaye, utapitia dhiki kubwa na mateso makubwa! Kukamilishwa silo jambo rahisi au jepesi. Angalau lazima uwe na imani ya Ayubu, au hata labda imani kubwa kuliko yake. Unapaswa kujua kwamba majaribu katika siku zijazo yatakuwa makubwa kuliko majaribu ya Ayubu, na kwamba lazima bado upitie kuadibu kwa muda mrefu. Je, hili ni jambo rahisi? Ikiwa ubora wa tabia yako hauwezi kuboreshwa, ikiwa uwezo wako wa kuelewa umepungukiwa, na ikiwa unajua kidogo sana, basi wakati huo hutakuwa na ushuhuda wowote, lakini badala yake utakuwa kichekesho, kitu cha Shetani kuchezea. Ikiwa huwezi kushikilia maono sasa, basi huna msingi hata kidogo na katika siku zijazo utatupwa! Hakuna sehemu ya njia ambayo ni rahisi kutembea, kwa hivyo usiichukulie kwa urahisi. Lipime hili kwa uangalifu sasa na ufanye maandalizi ili uweze kuitembea vizuri sehemu ya mwisho ya njia hii. Hii ndiyo njia ambayo lazima itembewe katika siku zijazo, njia ambayo lazima watu wote waitembe. Lazima usikose kusikiliza maarifa haya; usifikirie kuwa kile Ninachokuambia si chote cha maana. Siku itakuja ambapo utayatumia vizuri—maneno

Yangu hayawezi kunenwa bure. Huu ndio wakati wa wewe kujiandaa, wakati wa kuandaa njia kwa ajili ya siku zijazo. Unapaswa kuandaa njia ambayo unapaswa kuitembea baadaye; unapaswa kuwa na hofu na wasiwasi kuhusu jinsi utakavyoweza kusimama imara katika siku zijazo na ujiandae vizuri kwa ajili ya njia yako ya baadaye. Usiwe mlafi na mvivu! Lazima ufanye kila kitu uwezacho kabisa kutumia muda wako vizuri, ili uweze kupata kila kitu unachohitaji. Ninakupa kila kitu ili uweze kuelewa. Umeona kwa macho yako mwenyewe kwamba katika kipindi kisichozidi miaka mitatu, Nimenena mambo mengi sana na kufanya kazi nyingi sana. Sababu moja ya Mimi kufanya kazi kwa njia hii ni kwamba watu wamepungukiwa sana, na sababu nyingine ni kwamba muda ni mfupi sana; hakuwezi kuwa na kuchelewa zaidi. Unadhani kuwa watu lazima kwanza waweze kupata ufahamu kamili wa ndani kabla ya kushuhudia na kutumiwa—lakini hiyo haitakuwa polepole sana? Kwa hivyo, Nitalazimika kuandamana na wewe kwa muda gani? Ukinilazimisha niandamane na wewe hadi nitakapozeeka na niwe na mvi, hilo halitawezekana! Kwa kupitia dhiki kubwa zaidi, ufahamu wa kweli ndani ya watu wote utatimizwa. Hizi ni hatua za kazi. Punde unapofahamu kikamilifu maono yaliyoshirikiwa leo na ufikie kimo cha kweli, basi ugumu wowote utakaopitia katika siku zijazo hautakushinda na utaweza kuustahimili. Nitakapokuwa nimemaliza hatua hii ya mwisho ya kazi na kumaliza kunena maneno ya mwisho, katika siku zijazo watu watahitajika kutembea njia yao wenyewe. Hili litatimiza maneno yaliyonenwa hapo awali: Roho Mtakatifu ana agizo kwa kila mtu, na kazi ya kufanya ndani ya kila mtu. Katika siku zijazo, kila mtu ataitembea njia anayopaswa kuitembea, akiongozwa na Roho Mtakatifu. Ni nani atakayeweza kuwatunza wengine huku akipitia dhiki? Kila mtu ana mateso yake mwenyewe, na kila mmoja ana kimo chake mwenyewe. Hakuna kimo cha mtu yeyote kilicho sawa na cha mtu mwingine yeyote. Waume hawataweza kuwatunza wake zao, au wazazi kuwatunza watoto wao; hakuna mtu atakayeweza kumtunza mtu mwingine yeyote. Haitakuwa kama sasa, wakati ambapo kutunzana na kuhimiliana bado kunawezekana. Huo utakuwa wakati ambapo mtu wa kila aina amefunuliwa. Yaani, Mungu anapowapiga wachungaji, basi kondoo wa kundi watatawanyika, na wakati huo ninyi hamtakuwa na kiongozi yeyote wa kweli. Watu watakuwa wamegawanyika—haitakuwa kama sasa, wakati ambapo mnaweza kukusanyika pamoja kama mkutano. Katika siku zijazo, wale ambao hawana kazi ya Roho Mtakatifu wataonyesha sura zao za kweli. Waume watawasaliti wake zao, wake watawasaliti waume zao, watoto watawasaliti wazazi wao, na wazazi watawatesa watoto wao—moyo wa binadamu ni usioeleweka kabisa! Kile kinachoweza kufanywa ni kwa mtu kushikilia tu kile mtu alichu nacho, na kuitembea vizuri sehemu ya mwisho ya njia. Sasa hivi, ninyi hamwoni hili wazi wazi; nyinyi nyote ni wasiofikiria mambo yajayo. Si jambo rahisi kupitia hatua hii ya kazi kwa mafanikio.

Wakati wa dhiki hautarefushwa sana; kwa kweli, utadumu kwa chini ya mwaka mmoja.

Ukidumu kwa mwaka mzima, hatua inayofuata ya kazi itacheleweshwa, na kimo cha watu hakitakuwa cha kutosha. Ukiwa mrefu sana, basi watu hatawaweza kuistahimili. Hata hivyo, kimo cha watu kina mapungufu yake. Baada ya kazi Yangu mwenyewe kukamilika, hatua inayofuata itakuwa kwa watu kuitembea njia wanayopaswa kuitembea. Kila mtu lazima aelewe ni njia gani anayopaswa kuitembea—ni njia na mchakato wa kuteseka, na pia ni njia ya kusafisha dhamira yako ya kumpenda Mungu. Unapaswa kuingia katika ukweli upi, ni ukweli gani unaopaswa kujazilia, jinsi unavyopaswa kupitia na unapaswa kuingia kutoka katika kipengele kipi—sharti uelewe mambo haya yote. Lazima ujiandae sasa. Dhiki itakapokujia, utakuwa umechelewa mno. Kila mtu lazima achukue mzigo kwa ajili ya maisha yake mwenyewe na usingojee kila wakati maonyo ya wengine au wengine kukuvuta na kukuelekeza kila wakati. Nimesema mengi sana lakini wewe bado hujui ni ukweli gani unaopaswa kuingia ndani au kujiandaa nao. Hili linaonyesha kuwa hujafanya jitihada kusoma maneno ya Mungu. Hubebi mzigo wowote kwa ajili ya maisha yako mwenyewe—hilo linawezaje kukubalika? Huelewi kile unachopaswa kuingia katika, huelewi kile unachopaswa kuelewa, na bado huna mwelekeo kuhusu ni njia gani ya baadaye unayopaswa kuchukua. Je, si wewe huna maana kabisa? Una maaana gani? Kile mnachofanya sasa ni kujenga na kuandaa njia zenu wenyewe. Lazima ujue ni nini ambacho watu wanapaswa kutimiza na lazima ujue kiwango cha mahitaji ya Mungu kwa wanadamu. Lazima uwe na ufahamu ufuatao: Haijalishi chochote, hata ingawa mimi ni mpotovu sana, lazima nifidie kasoro hizi mbele za Mungu. Kabla Mungu hajaniambia, sikuelewa, lakini sasa kwa kuwa Ameniambia na ninaelewa, lazima niharakishe kufidia upungufu huo, kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida, na kuishi kwa kudhihirisha taswira inayoweza kuyaridhisha mapenzi ya Mungu. Hata kama siwezi kufikia kile ambacho Petro alifanya, angalau lazima niishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida. Kwa njia hii, naweza kuuridhisha moyo wa Mungu.

Sehemu ya mwisho ya njia hii itaongezeka kutoka sasa hadi mwisho wa dhiki ya baadaye. Sehemu hii ya njia itakuwa wakati ambapo kimo cha kweli cha watu kinafichuliwa na vile vile kuonyesha ikiwa wana imani ya kweli au la. Kwa sababu sehemu hii ya njia itakuwa njia ngumu na yenye mabonde zaidi kuliko ile ambayo watu wameongozwa kwayo hapo awali, inaitwa “sehemu ya mwisho ya njia.” Ukweli ni kwamba siyo sehemu ya mwisho kabisa ya njia; hii ni kwa sababu baada ya kupitia dhiki, baadaye utapitia kazi ya kueneza injili na kutakuwa na sehemu ya watu ambao watapitia kazi ya kutumiwa. Kwa hivyo “sehemu ya mwisho ya njia” inazungumziwa tu kwa kurejelea dhiki ya kuwasafisha watu na kwa mazingira magumu. Kwenye sehemu hiyo ya njia ambayo ilitembewa zamani, Mimi binafsi nilikuongoza kwenye safari hiyo ya furaha, Nikikushika mkono kukufundisha, na kukulisha kutoka katika kinywa Changu mwenyewe. Ingawa umepitia hukumu na kuadibu mara nyingi, vimekuwa tu mapigo

mepesi kuhusiana na wewe. Bila shaka, hilo limesababisha mitazamo yako juu ya imani yako kwa Mungu ibadilike kwa kiasi kikubwa; pia imesababisha tabia yako kuimarika kwa kiasi kikubwa, na imekuruhusu upate ufahamu mdogo kunihusu. Lakini Ninachosema ni kwamba wakati watu walikuwa wakiitembea sehemu hiyo ya njia hiyo, juhudi angalifu au gharama zilizolipwa na watu zilikuwa ndogo kiasi—ni Mimi ndimi nimekuongoza hadi pale ulipo leo. Hii ni kwa sababu Sikuhitaji ufanye kitu chochote; kwa kweli, matakwa Yangu kwako si ya juu hata kidogo—Ninakuruhusu tu uchukue kile kinachopatikana. Katika kipindi hiki cha muda Nimewapa mahitaji yenu bila kukoma na Sijawahi kuwawekea madai yasiyotimizika. Mmepitia kuadibu kwa kurudiwa, lakini hamjatimiza mahitaji Yangu ya asili. Mnarudi nyuma na mnakata tamaa, lakini Mimi sizingatii hili kwa sababu sasa ndio wakati wa kazi Yangu binafsi, na sichukulii “ibada” yako Kwangu kwa uzito sana. Lakini kwenye njia kuanzia sasa kuendelea, Sitafanya kazi au kunena tena na wakati utakapokuja Sitawaacha muendelea tena kwa njia ya uzembe namna hiyo. Nitawaruhusu mpate mafunzo mengi ya kujifunza na Sitawaruhusu mchukue kile kinachopatikana. Kimo halisi mlichu nacho leo lazima kifunuliwe. Ikiwa juhudi zenu za miaka mingi zimezaa matunda mwishowe au la itaonekana katika jinsi mnavyoitembea sehemu hii ya mwisho ya njia. Hapo zamani, mlidhani kwamba kumwamini Mungu lilikuwa jambo rahisi sana na hiyo ilikuwa kwa sababu Mungu hakuwa Akikutendea kwa ukali. Na sasa, je? Je, mnafikiri kwamba kumwamini Mungu ni rahisi? Je, bado mnahisi kuwa kumwamini Mungu kunawafanya muwe na furaha na wachangamfu kama watoto wanaocheza mitaani? Ni kweli kwamba ninyi ni kondoo; hata hivyo, lazima muweze kuitembea njia mnayopaswa kuitembea ili kulipa rehema ya Mungu, na kumpata kikamilifu Mungu mnayemwamini. Msijidhihaki na msijidanganye! Ikiwa unaweza kuendelea kwenye sehemu hii ya njia, basi utaweza kuona tukio ambalo halijawahi kuonekana hapo awali la kazi Yangu ya injili kuenea katika ulimwengu mzima, na utakuwa na bahati nzuri ya kuwa mwandani Wangu na kufanya wajibu wako katika kupanua kazi Yangu katika ulimwengu mzima. Wakati huo, utaendelea kwa furaha kuitembea njia unayopaswa kuitembea. Siku za usoni zitang’aa bila kikomo, lakini jambo la msingi sasa ni kuitembea vizuri sehemu hii ya mwisho ya njia. Lazima utafute na uandae jinsi ya kufanya hivi. Hili ndilo lazima ufanye sasa; hili ni suala muhimu sasa!

Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani III (Julai 1993 hadi Machi 1994)

Unapaswa Kushughulikiaje Wito Wako wa Baadaye?

Je, unaweza kuwasilisha tabia inayoonyeshwa na Mungu katika kila enzi kwa njia thabiti, kwa lugha inayowasilisha umuhimu wa enzi hiyo kwa njia inayofaa? Je, wewe unayepitia kazi ya Mungu ya siku za mwisho unaweza kueleza tabia ya Mungu yenye haki kwa utondoti? Je,

unaweza kushuhudia kuhusu tabia ya Mungu kwa uwazi na usahihi? Utawezaje kupitisha kile ambacho umeona na kupitia kupitia kwa maskini hawa wa kuhurumiwa, na waumini wa kidini wa kumcha Mungu waliojitolea na waliojawa na njaa na kiu ya haki na wanaongoja uwe mchungaji wao? Ni watu wa aina gani ndio wanangoja uwe mchungaji wao? Unaweza kuwaza kweli? Je, unajua mzigo ulio begani mwako, kazi yako na majukumu yako? Hisia yako ya kihistoria ya mwito iko wapi? Utahudumu vipi kama kiongozi mzuri wa wakati unaofuata? Je, unao hisia nzuri ya uongozi? Utaeleza mkuu wa kila kitu kama nini? Je, ni mkuu wa kila kitu kilicho hai na viumbe vyote duniani? Una mipango ipi ya kuendelea kwa hatua inayofuata ya kazi? Ni watu wangapi ndio wanangoja uwe mchungaji wao? Je, jukumu lako ni nzito? Wao ni masikini, wa kuhurumiwa, vipofu na waliopotea na wanalia gizani, “Njia iko wapi?” Jinsi gani wanatamani mwangaza, kama nyota iangukayo kutoka angani, ianguke ghafla na kutawanya nguvu za giza zilizowakandamiza wanadamu kwa miaka mingi. Ni nani anayeweza kujua jinsi wanavyotumaini kwa hamu, na wanavyotamani hili usiku na mchana? Wanadamu hawa wanaoteseka mno wamebaki wafungwa katika jela za giza, bila tumaini la kuwachiliwa huru, hata ile siku ambayo mwanga utaonekana; ni lini hawatalia kwa uchungu tena? Roho hizi dhaifu ambao kamwe hazijapewa pumziko kwa hakika zinateseka na bahati hii mbaya. Kwa muda mrefu wamefungiwa nje na kamba zisizo na huruma na historia iliyokwama katika wakati. Ni nani amewahi kusikia sauti ya vilio vyao? Ni nani amewahi kuona nyuso zao zenye taabu? Umewahi kufikiria jinsi moyo wa Mungu ulivyosononeka na ulivyo na wasiwasi? Anawezaje kustahimili kuona mwanadamu asiye na hatia, Aliyemuumba kwa mikono Yake Mwenyewe akiteswa na makali? Mwishowe, wanadamu ndio wasio na bahati na waliopewa sumu. Hata ingawa wamenusurika mpaka siku hii, ni nani angefikiri kuwa wamepewa sumu na yule mwovu kwa muda mrefu? Je, umesahau kuwa wewe ni mmoja wa waathiriwa? Kwa ajili ya upendo wako kwa Mungu, una nia ya kufanya kila uwezalo kuwaokoa walionusurika? Je, huna nia, ya kutumia nguvu zako zote kulipiza Mungu anayempenda binadamu kama nyama na damu Yake Mwenyewe? Unaitafsiri vipi hali ya kutumiwa na Mungu kuishi maisha yako yasiyo ya kawaida? Je, unao kweli uamuzi na matumaini ya kuishi kwa kudhihirisha maisha ya maana ya mtu mcha Mungu anayemtumikia Mungu?

Kusudi la Kuwasimamia Binadamu

Ikiwa watu wanaweza kweli kuiona vizuri njia sahihi ya maisha ya binadamu na vilevile kusudi la usimamizi wa Mungu wa binadamu, wasingeshikilia mategemeo yao ya baadaye na majaliwa yao binafsi kama hazina mioyoni mwao. Kisha wasingetataka tena kuwatumikia wazazi wao, ambao ni wabaya zaidi kuliko nguruwe na mbwa. Je, mustakabali na majaliwa ya mwanadamu si hasa wale wanaodaiwa kuwa “wazazi” wa Petro wa wakati wa sasa? Yamekuwa tu kama mwili na damu ya mwanadamu. Je, hatima na mustakabali wa mwili utakuwa upi hasa?

Je, utakuwa kumwona Mungu wakati ukiwa ungali hai, au kwa roho kukutana na Mungu baada ya kifo? Je, kesho mwili utaishia katika tanuu kuu ya taabu, au katika moto mkubwa? Je, si maswali kama haya yanahusu iwapo mwili wa mwanadamu utahimili taabu au utavumilia habari kubwa sana ambayo kila mtu aliye katika mkondo huu wa sasa ambaye ana akili na ni mwenye busara anayahangaika? (Hapa, kuteseka kunarejelea kupokea baraka; kunamaanisha kwamba majaribu ya siku zijazo ni yenye manufaa kwa hatima ya mwanadamu. Taabu hurejelea kushindwa kusimama imara, au kudanganywa; au, kunamaanisha kwamba mtu atakumbana na hali za bahati mbaya na kupoteza maisha ya mtu katikati ya majanga, na kwamba hakuna hatima nzuri kwa roho wa mtu.) Ingawa wanadamu wana mantiki timamu, pengine kile wanachofikiri hakifanani kabisa na kile ambacho mantiki yao yanapaswa kuwa nacho. Hii ni kwa sababu wote ni waliochanganyikiwa na wao hufuata vitu bila kufikiri. Wote wanapaswa kuwa na ufahamu wa kina wa kile ambacho wanapaswa kuingia kwacho, na kwa mahususi wanapaswa kutatua kile wanachopaswa kuingia kwacho wakati wa mateso (yaani, wakati wa utakasaji katika tanuu), na vile vile kile wanachopaswa kujiandaa nacho wakati wa majaribu ya moto. Usiwatumikie wazazi wako siku zote (kumaanisha mwili) ambao ni sawa na nguruwe na mbwa na hata ni wabaya zaidi kuliko chungu na wadudu. Kuna haja gani ya kuteseka juu ya hilo, kufikiri sana, na kupiga bongo zako? Mwili si wako, bali upo katika mikono ya Mungu, ambaye kando na kukudhibiti wewe, pia Anamwamuru Shetani. (Hili linamaanisha kuwa kiasili mwili ni wa Shetani. Kwa kuwa Shetani pia yumo mikononi mwa Mungu, inaweza tu kusemwa hivi. Hii ni kwa sababu inashawishi zaidi kusema namna hiyo; inamaanisha kuwa wanadamu hawamilikiwi na Shetani kabisa, bali wamo mikononi mwa Mungu.) Unaishi chini ya mateso ya mwili, lakini, je, mwili ni wako? Uko chini ya udhibiti wako? Kwa nini upige bongo sana juu ya hilo? Kwa nini usumbuke sana kumsihi Mungu kwa ajili ya mwili wako uliooza ambao umeshahukumiwa zamani sana, kulaaniwa na vilevile kutiwa najisi na roho wachafu? Kuna haja gani ya kuwaweka washirika wa Shetani karibu sana na moyo wako? Huna wasiwasi kwamba mwili unaweza kuuharibu mustakabali wako halisi, matumaini yako mazuri, na hatima ya kweli ya maisha yako?

Njia ya leo si rahisi kuitembea. Inaweza kusemekana kwamba ni vigumu kuipata, na katika enzi zote imekuwa adimu sana. Hata hivyo, nani angeweza kufikiria kuwa mwili wa mwanadamu pekee ungetosha kumwagamiza? Kazi ya leo hakika ni ya thamani kama vile mvua ya majira ya kuchipua na ni ya thamani kama wema wa Mungu kwa mwanadamu. Hata hivyo, ikiwa mwanadamu hajui kusudi la kazi Yake ya sasa au kuelewa kiini cha mwanadamu, basi inawezekanaje tunu na thamani yake vizungumziwe? Mwili si wa wanadamu wenyewe, hivyo kwa kweli hakuna mtu anayeweza kuona waziwazi hatima yake itakuwa wapi. Hata hivyo, unapaswa kujua vizuri kwamba Mungu wa uumbaji Atawarudisha binadamu, ambao waliumbwa, katika nafasi yao ya asili, na kurejesha sura yao ya asili kutoka wakati wa kuumbwa

kwao. Atachukua tena kikamilifu pumzi Aliyoipuliza ndani ya binadamu, na kuchukua tena mifupa na mwili wake na kurudisha vyote kwa Bwana wa viumbe. Atabadilisha na kufanya upya binadamu kikamilifu, na kuchukua tena kutoka kwa binadamu urithi wote wa Mungu ambao si wa binadamu, bali ni wa Mungu, na kamwe hatampa tena binadamu urithi huo. Hii ni kwa sababu kiasili, hakuna hata kitu kimoja kati ya hivyo kilichokuwa cha binadamu. Atavichukua vyote tena—huu si uporaji usio wa haki; lakini badala yake, unakusudiwa kuirejesha mbingu na dunia katika hali zake za asili, na vile vile kubadilisha na kumfanya upya binadamu. Hii ndiyo hatima inayofaa kwa mwanadamu, ingawa pengine haitakuwa kutwaa tena kwa mwili baada ya kuadibiwa, kama watu wanavyoweza kufikiri. Mungu hataki mifupa ya mwili baada ya maangamizi yake; Anataka vitu vya asili katika mwanadamu ambavyo mwanzo vilikuwa vya Mungu. Hivyo, Hatawaangamiza binadamu au kuuondoa kabisa mwili wa mwanadamu, kwa kuwa mwili wa mwanadamu si mali yake binafsi. Badala yake, ni kiungo cha Mungu, ambaye anasimamia binadamu. Angewezaje kuuangamiza mwili wa mwanadamu kwa ajili ya “furaha” Yake? Kufikia sasa, je, umeachana kwa kweli na ukamilifu wa huo mwili wako ambao hauna thamani hata ya senti moja? Kama ungeweza kuelewa asilimia thelathini ya kazi ya siku za mwisho (hii asilimia ndogo thelathini inamaanisha kuifahamu kazi ya Roho Mtakatifu leo na vile vile kazi ya Mungu ya neno katika siku za mwisho), basi usingeweza kuendelea “kuutumikia” au “kuwa” na upendo kwa mwili wako—mwili ambao umepotoka kwa miaka mingi—kama ilivyo leo. Unapaswa kuona wazi wazi kwamba binadamu sasa wameendelea hadi kufikia hali ambayo haijawahi kufikiwa na hawataendelea tena kusonga mbele kama magurudumu ya historia. Mwili wako ulioota kuvu umeshafunikwa na nzi tangu zamani, hivyo unawezaje kuwa na nguvu ya kurudisha nyuma magurudumu ya historia ambayo Mungu ameyawezesha kuendelea hadi siku hii ya leo? Unawezaje kufanya saa ipigayo kimya kimya ya siku za mwisho ipige tena, na iendeleo kusogeza mikono yake kwa upande wa kulia? Unawezaje kuabadilisha upya ulimwengu ambao unaonekana kama umefunikwa na ukungu mzito? Je, mwili wako unaweza kuifufua milima na mito? Je, mwili wako, ambao una kazi kidogo tu, unaweza kweli kurejesha aina ya ulimwengu wa binadamu ambao umekuwa ukiutamani sana? Unaweza kweli kuwaelimisha wazawa wako wawe “binadamu”? Je, unaelewa sasa? Mwili wako unamilikiwa na nini hasa? Makusudi asili ya Mungu ya kumwokoa mwanadamu, ya kumkamilisha mwanadamu, na ya kumbadilisha mwanadamu hayakuwa kukupatia nchi nzuri ya asili au kuleta pumziko la amani kwa mwili wa mwanadamu; ilikuwa ni kwa ajili ya utukufu Wake na ushuhuda Wake, kwa furaha bora ya binadamu hapo baadaye, na ili kwamba hivi karibuni waweze kupumzika. Bado, ilikuwa kwa ajili ya mwili wako, maana mwanadamu ni mtaji wa usimamizi wa Mungu, na mwili wa mwanadamu ni kiungo tu. (Mwanadamu ni kitu chenye roho na mwili, ilhali mwili ni chombo kiozacho tu. Hii humaanisha kwamba mwili ni chombo cha kutumiwa katika mpango wa usimamizi.) Unapaswa kujua kwamba Mungu kuwakamilisha, kuwatimiza, na kuwapata

wanadamu hakuleti kitu chochote ila panga na maangamizi juu ya miili wao, na na vile vile mateso yasiyokoma, moto mkali, hukumu zisizokuwa na huruma, kuadibu, laana, na majaribu yasiyokuwa na mipaka. Hicho ni kisa cha ndani na ukweli wa kazi ya kumsimamia binadamu. Hata hivyo, vitu hivi vyote vinalengwa kwa mwili wa mwanadamu, na mishale yote ya uhasama bila huruma inaelekezwa kwenye mwili wa mwanadamu (kwa maana mwanadamu hana hatia). Haya yote ni kwa ajili ya utukufu na ushuhuda Wake, na kwa ajili ya usimamizi Wake. Hii ni kwa sababu kazi Yake si kwa ajili ya binadamu tu, bali pia kwa ajili ya mpango wote, na vile vile kutimiza mapenzi Yake ya asili Alipomuumba binadamu. Kwa hiyo, pengine asilimia tisini ya kile ambacho mwanadamu hupitia kinajumuisha mateso na majaribu ya moto, na kuna siku chache sana ambazo ni tamu na zenye furaha au hata hakuna kabisa, ambazo mwili wa mwanadamu umekuwa ukitamani sana. Sembuse mwanadamu kuweza kufurahia nyakati za furaha katika mwili, akishinda nyakati nzuri pamoja na Mungu. Mwili ni mchafu, hivyo kile ambacho mwili wa mwanadamu unakiona au unakifurahia ni kuadibu kwa Mungu tu ambako mwanadamu huona kukiwa kusiko kuzuri, na ni kana kwamba hakuna mantiki ya kawaida. Hii ni kwa sababu Mungu atadhihirisha tabia Yake ya haki, ambayo haipendwi na mwanadamu, haivumilii makosa ya mwanadamu, na huchukia kabisa maadui. Mungu hufichua waziwazi tabia Yake yote kwa njia yoyote inayolazimu, na hivyo Akihitimisha kazi ya vita Vyake na Shetani vya miaka elfu sita—kazi ya wokovu wa binadamu wote na maangamizo ya Shetani wa zamani!

Asili na Utambulisho wa Mwanadamu

Kwa kweli, Waisraeli hawajasikitika, wameing'amua kazi ambayo inafanywa na Mungu kwa miaka elfu sita, mpaka hivi sasa, kwa kuwa Sikuwaacha. Badala yake, kwa sababu mababu zao walikula tunda kutoka kwa mti wa ujuzi wa mema na maovu lililotolewa na yule mwovu, waliniacha kwa ajili ya dhambi. Mema ni Yangu, wakati maovu ni ya yule mwovu ambaye hunirairai kwa ajili ya dhambi. Mimi Simlaumu mwanadamu, wala Simwangamizi kwa ukatili au kumtolea kuadibu kusiko na huruma, kwani uovu haukuwa wa wanadamu kiasili. Kwa hivyo ingawa wale Waisraeli walinipigilia misumari msalabani hadharani, wao, ambao wamekuwa wanamngoja Masiha na Yehova na kumtamani sana Mwokozi Yesu, hawajasahau ahadi Yangu. Hii ni kwa sababu Sijawatelekeza. Hata hivyo, Nilikuwa nimechukua damu kama ushahidi wa agano Nililoanzisha na mwanadamu. Ukweli huu umekuwa agano la damu lililoandikwa katika mioyo ya watu wachanga na wasio na hatia, kana kwamba lilichapiliwa, na kama kuishi kwa pamoja kwa amani kwa mbingu na dunia milele. Sijawahi kuzidanganya nafsi hizo za huzuni Nilizojiokoa, kuzipata, na ambazo hunipenda zaidi ya yule mwovu baada ya Mimi kuzijaalia na kuzichagua. Kwa hiyo, kwa shauku zinatazamia kurudi Kwangu na kwa hamu zinatarajia kukutana na Mimi. Kwa kuwa Sijawahi kufuta agano Nililoanzisha nazo kwa damu, si ajabu kwamba zimekuwa zikisubiri kwa hamu. Nitawateka tena wanakondoo hawa ambao wamepotea

kwa miaka, kwa maana siku zote Nimewapenda mwanadamu. Ni kwamba tu dalili za uovu zimeongezwa kwa wema katika wanadamu. Nitazipata zile nafsi hafifu ambazo zinanipenda na ambazo Nimezipenda tayari, lakini Nawezeje kuwaleta wale waovu ambao hawajawahi kunipenda na wametenda kama adui ndani ya nyumba Yangu? Sitawaleta wazawa wa Shetani na nyoka mwenye sumu kali ambao hunichukia, hunipinga, hunikataa, hunishambulia, na kunilaani ndani ya ufalme Wangu, hata ingawa Nimeanzisha agano la damu na mwanadamu. Unapaswa kujua kwa nini na kwa ajili ya nani Ninatekeleza kazi hiyo. Je, ni wema au uovu katika upendo wako? Je, kwa kweli unanijua kama vile walivyonijua Daudi na Musa? Je, kwa kweli unanihudumia kama vile alivyonihudumia Ibrahimu? Ni kweli kwamba unafanywa kamili na Mimi, lakini unapaswa kujua ni nani utakayemwakilisha na ni nani utakayekuwa na matokeo sawa na. Katika maisha yako, una mavuno ya furaha na mengi katika kupata uzoefu wa kazi Yangu? Je, ni mengi na yenye matokeo mazuri? Unapaswa kujichunguza mwenyewe. Kwa miaka umefanya kazi kwa bidii kwa ajili Yangu, lakini umewahi kupata chochote? Umebadili au kupata kitu chochote? Badala ya uzoefu wako katika shida, je, unakuwa kama Petro ambaye alisulubiwa, au kama Paulo ambaye alibwagwa na kupokea mwanga mkubwa? Unapaswa kuwa na ufahamu wa haya. Mimi sizungumzi siku zote juu ya, na kufikiria kuhusu maisha yako ambayo ni madogo kuliko mbegu ya haradali, ambayo ni ukubwa wa punje ya mchanga. Kusema kweli, ni mwanadamu ambaye Ninasimamia. Hata hivyo, Sifikirii maisha ya mwanadamu, ambaye wakati mmoja Nilimchukia lakini baadaye Nikamwinua tena, kama sehemu muhimu ya usimamizi Wangu. Unapaswa kuwa mwenye uhakika juu ya utambulisho wako wa zamani kwa kweli ulikuwa upi, na ni nani mliyemtumikia kama watumwa. Kwa hiyo, Situmii nyuso za wanadamu kama ya Shetani kama mali ghafi kuwasimamia, kwa kuwa wanadamu si vitu vya thamani. Mnapaswa kukumbuka mtazamo Wangu kwenu hapo mwanzoni, na hotuba Yangu kwenu wakati huo ambayo haikuwa bila umuhimu wa utendaji. Unapaswa kujua kwamba zile “kofia” juu ya vichwa vyenu zina msingi. Ninadhani kwamba nyote mnajua kwamba hamkuwa wa Mungu kwa asili, lakini mlikamatwa na Shetani zamani na kutumikia nyumbani kwake kama watumishi waaminifu. Mmenisahau kwa muda mrefu, kwani kwa muda mrefu mmekuwa nje ya nyumba Yangu lakini mikononi mwa yule mwovu. Wale ambao Mimi huokoa ni wale ambao Nimewaamulia kabla zamani na wamekombolewa na Mimi, wakati ninyi ni nafsi hafifu ambazo zimewekwa kati ya wanadamu kama jambo la pekee. Mnapaswa kujua kwamba nyinyi si wa nyumba ya Daudi au Yakobo, lakini ni wa nyumba ya Moabu, ambao ni wanachama wa kabila la Mataifa. Kwa maana Sikuanzisha agano na nyinyi, lakini Nilitekeleza tu kazi na kunena kati yenu, na kuwaongoza. Damu Yangu haikumwagika kwa ajili yenu. Nilitekeleza tu kazi kati yenu kwa ajili ya ushuhuda Wangu. Je, hamjajua hilo? Je, kazi Yangu kweli ni kama Yesu kumwaga damu hadi kufa kwa niaba yenu? Haikuwa na thamani kwamba Nilivumilia fedheha kubwa kwa ajili yenu. Mungu, ambaye hana dhambi kabisa, Alikuwa moja kwa moja kwa pahali

panapochukiza na kukirihi kabisa, dunia ya nguruwe na mbwa ambayo haikufaa kwa binadamu kuishi, lakini bado Nilivumilia hii aibu yote ya ukatili kwa ajili ya utukufu wa Baba Yangu na kwa ajili ya ushuhuda wa milele. Mnapaswa kujua mienendo yenu na kuona kwamba nyinyi si watoto waliozaliwa katika “familia tajiri na yenye nguvu” bali watoto fukara tu wa Shetani. Nyinyi si waanzilishi kati ya wanadamu, na hamna haki za kibinadamu au uhuru. Kwa asili, hamkuwa na mgao wowote kabisa la baraka kutoka kwa binadamu au ufalme wa mbinguni. Hili ni kwa sababu mko chini kabisa ya binadamu katika wanadamu, na Sijawahi kufikiria kuhusu wakati wenu ujao. Kwa hivyo, ingawa ilikuwa sehemu ya asili ya mpango Wangu kwamba leo Ningekuwa na imani kuwakamilisha, ni kazi ya pekee, kwa sababu hadhi yenu ni ya chini sana na kiasili hamkuwa na mgawo katika binadamu. Je, hii si baraka kwa wanadamu?

Wale Ninaowaokoa ni nafsi ambazo Nilizitoa kutoka toharani zamani, na waliochaguliwa ambao Nilitembelea zamani, kwa kuwa wametamani sana kuonekana Kwangu tena kati yao. Wamenipenda, na wameandika agano Langu ambalo Nilianzisha kwa damu katika mioyo yao, kwa sababu Nimewapenda. Wao ni kama kondoo waliopotea ambao wamekuwa wakinitafuta kwa miaka mingi, na wao ni wazuri, na kwa hivyo Ninawaita Waisraeli wazuri na malaika wadogo wanaopendeza. Singepitia aibu kama hii iwapo Ningekuwa miongoni mwao. Ni kwa sababu wananipenda zaidi kuliko wanavyopenda maisha yao wenyewe, na Ninawapenda kama kile ambacho ni kirembo zaidi kati ya vitu vyote. Ni kwa sababu waliumbwa na Mimi na ni Wangu; hawajawahi kunisahau. Upendo wao unazidi upendo wenu, na wananipenda kwa upendo mkubwa zaidi kuliko mnavyopenda maisha yenu wenyewe. Wananitii Mimi kama vile njiwa wadogo weupe hufanyia anga, na kwa upendo mkubwa zaidi kuliko mnavyonifanyia. Na ni kwa sababu wao ni wazawa wa Yakobo, watoto wa Adamu, na ni miongoni mwa wateule Wangu, kwa kuwa Nimewapenda zamani, na hata zaidi kuliko Ninavyowapenda, na kwa sababu nyinyi ni waasi sana, upinzani wenu ni mkubwa sana, mnaniangalia kwa dharau sana, hamnithamini hata kidogo Kwangu, mnanipenda kidogo sana, na mnanichukia sana. Mnadharau kazi Yangu, na kutweza vitendo Vyangu sana. Tofauti na wao, hamjawahi kuona matendo Yangu kuwa kitu cha thamani. Badala yake, mnayadharau na macho mekundu ya wasiwasi, kama tu Shetani. Utiifu wenu uko wapi? Tabia zenu ziko wapi? Upendo wenu uko wapi? Ni lini mmeonyesha wazi dalili ya upendo ndani yenu? Ni lini mmechukua kazi Yangu kwa uzito kabisa? Hurumia wale malaika wa kupendeza ambao kwa wasiwasi wananitazamia na kuteseka sana wakati wanaponisubiri kwa wasiwasi, kwani Ninawapenda kwa dhati. Hata hivyo, kile Ninachokiona leo ni ulimwengu usio wa kibinadamu sana ambao hauhusiani nao. Je, hamfikirii kuwa dhamiri zenu zilikuwa zisizojali na zisizo na huruma muda mrefu uliopita? Je, hamfikirii kuwa nyinyi ndio watu duni mnaozuia kurudiana Kwangu na malaika wa kupendeza? Ni lini hawajakuwa wakisubiri kurudi Kwangu? Ni lini hawajakuwa wakisubiri kuungana tena na Mimi? Je, ni lini hawajatarajia kushinda kwa

siku nzuri na kula pamoja na Mimi? Je, mliwahi kutambua kile mfanyacho leo—yaani, kufanya ghasia ulimwenguni, kupanga njama dhidi ya nyinyi kwa nyinyi, kudanganyana, kutenda kwa uongo, kwa siri na kwa ukavu wa macho, kutojua ukweli, kuwa wasio waaminifu na wadanganyifu, kutenda ubembelezaji, nyinyi kujiona daima kuwa waadilifu na bora zaidi kuliko wengine, kuwa wenye kiburi, na kutenda kikatili kama wanyama wa mwitu milimani na kwa fujo kama mfalme wa wanyama—huu ndio mfano wa mwanadamu? Nyinyi ni fidhuli na wasio na busara. Hamjawahi kuliona neno Langu kuwa hazina, lakini badala yake mmechukua mtazamo wa dharau. Kwa njia hii, mafanikio, maisha ya kweli ya binadamu, na matumaini mazuri yangetoka wapi? Je, wazo lako badhirifu litakuokoa kwa kweli kutoka kwa kinywa cha chui? Kweli litakuokoa kutoka kwa moto unaowaka? Je, ungekuwa umeanguka hadi hapa iwapo kwa kweli ungeiona kazi Yangu kuwa kitu cha thamani kubwa mno? Inaweza kuwa kwamba majaliwa yako kweli hayawezi kubadilishwa? Je, uko tayari kufa na majuto kama haya?

Utambulisho wa Asili wa Mwanadamu na Thamani Yake: Je, Viko Namna Gani?

Mlitengwa kutoka kwa matope na kwa vyovyote vile, mlichaguliwa kutoka kwa mashapo, wachafu na mliochukiwa na Mungu. Mlikuwa wa Shetani na wakati mmoja mlikanyagwa na kuchafuliwa na yeye. Hii ndiyo maana inasemwa kuwa mlitengwa kutoka kwa matope, na nyinyi si watakatifu, lakini badala yake nyinyi ni vitu visivyo binadamu ambavyo Shetani kwa muda mrefu alikuwa amevifanya vipumbavu. Haya ndiyo maelezo sahihi zaidi yenu. Lazima mtambue kuwa nyinyi ni uchafu unaopatikana katika maji yaliyotuama na matope, kinyume na ushikaji unaofaa kama samaki na uduvi, kwa maana hakuna starehe inayoweza kupatikana kutoka kwenu. Kuzungumza waziwazi, nyinyi ni wanyama wa chini sana wa tabaka la chini zaidi, wanyama wabaya zaidi kuliko nguruwe na mbwa. Kusema kweli, kuwahutubia kwa istilahi kama hizo si chuku au kutia chumvi, lakini ni njia ya kurahisisha suala hilo. Kuwahutubia kwa istilahi kama hizo kwa kweli ni njia ya kuwapa heshima. Utambuzi wenu, hotuba, mwenendo kama watu, na vitu yote katika maisha yenu—ikiwa ni pamoja na hali yenu katika matope—vinatosha kuthibitisha kwamba utambulisho wenu ni “wa kipekee.”

Wale Wasiojifunza na Wanaosalia Wajinga: Je, Wao Sio Wanyama?

Unapoitembea njia ya leo, ufuatiliaji unaofaa zaidi ni wa aina gani? Katika ufuatiliaji wako, unapaswa kujiona kama mtu wa aina gani? Unafaa kujua jinsi unavyopaswa kukabili yote yanayokukumba leo, yawe majaribu ama taabu, ama kuadibu na laana isiyo ya huruma. Unapaswa kuyazingatia kwa uangalifu katika hali zote. Mbona Nasema hili? Nasema hili kwa

sababu yanayokukumba leo hata hivyo ni majaribu mafupi yanayotokea tena na tena; huenda huyaoni kuwa yanayosumbua sana kiakili, na hivyo unayaacha mambo yaende mrama, na huyachukulii kuwa rasilimali ya thamani katika ufuatiliaji wa maendeleo. Wewe ni asiyejali kweli! Sana kiasi kwamba unaifikiria rasilimali kana kwamba ni wingu linaloelea machoni pako, na huyathamini haya mapigo makali yanayokuja mara kwa mara—mapigo ambayo ni ya muda mfupi na yanayoonekana kuwa dhaifu kwako—ila unayatazama kwa utulivu, usiyafikirie kwa dhati na kuyachukulia tu kama mapigo ya mara moja. Wewe ni mfidhuli sana! Kwa mashambulio haya makali, mashambulio yaliyo kama dhoruba na yanayokuja mara kwa mara unaonyesha kupuuza kwa dharau; wakati mwingine hata unatabasamu bila hisia, ukifichua jinsi usivyojali—kwani hujawahi kujiwazia mbona unashinda ukipitia “misiba” kama hii. Je, Namtendea mwanadamu bila haki kwa kiasi kikubwa? Je, Natafuta makosa kwako? Ingawa shida zako za akili huenda zisiwe nzito jinsi Nilivyoeleza, kupitia utulivu wako wa nje, tangu zamani umebuni taswira nzuri sana ya dunia yako ya ndani. Hakuna maana ya Mimi kukuambia kwamba jambo la pekee lililofichika katika vina vya moyo wako ni matusi yasiyo adilifu na athari dhaifu ya huzuni ambayo wengine hawayaoni. Kwa sababu unahisi kwamba si haki hata kidogo kupitia majaribu kama haya, unatoa matusi; majaribu hayo hukufanya uhisi ukiwa wa dunia, na kwa sababu ya hili, unajawa na ghamu. Badala ya kutazama nidhamu na mapigo haya yanayorudiwa kama ulinzi bora kabisa, unayaona kuwa uchokozi wa Mbinguni usio na sababu, ama vinginevyo kama adhabu inayokufaa. Wewe ni mpumbavu sana! Unazifungia nyakati nzuri gizani bila huruma; mara kwa mara unaona nidhamu na mapigo mazuri kuwa mashambulio kutoka kwa adui zako. Huwezi kubadilika kulingana na mazingira yako sembuse kutaka kufanya hivyo kwani huna hiari ya kupata chochote kutoka kwa kuadibu huku kunakorudiwa na unakoona kuwa katili. Hufanyi juhudi yoyote kutafuta au kuchunguza, na, unajikabidhi tu kwa yale majaaliwayako, kwenda pahali popote itakapokuelekeza. Yanayoonekana kwako kuwa marudio makali hayajabadili moyo wako wala hayajatwaa udhibiti wa moyo wako; badala yake, yanakuchoma moyoni. Unaona “kuadibu huku katili” kuwa adui wako katika maisha haya tu na hujapata chochote. Wewe unajidai sana! Ni mara chache ambapo unaamini kwamba unapitia majaribu kama haya kwa sababu wewe ni duni sana; badala yake, unajiona aliye na bahati mbaya sana, na kusema kwamba Mimi daima hutafuta makosa kwako. Kufikia leo, kwa kweli una kiasi kipi cha maarifa ya kile Ninachosema na kufanya? Usifikiri kwamba una kipaji cha asili, uliye chini kidogo ya mbingu lakini juu sana ya dunia. Wewe si mwerevu zaidi kuliko mtu mwingine yeyote—na hata inaweza kusemwa kwamba wewe ni mpumbavu zaidi kuliko watu wowote duniani walio na mantiki, kwani unajiona sana kuwa bora, na hujawahi kujiona kuwa mtu wa chini; inaonekana kwamba unayachunguza matendo Yangu kwa utondoti kabisa. Kwa kweli, wewe ni mtu ambaye kimsingi hana mantiki, kwa kuwa hufahamu kabisa Nitakachofanya sembuse kutambua Ninachofanya sasa. Kwa hivyo Nasema kwamba wewe hata

hulingani na mkulima mzee anayefanya kazi kwa bidii shambani, mkulima ambaye hafahamu maisha ya binadamu hata kidogo na bado anategemeabaraka za Mbinguni wakati anapolima shamba. Huyafikirii maisha yako hata kidogo, hujui chochote chenye sifa sembuse kujijua. Wewe “una hadhi ya juu” sana! Kweli, Nawaonea ninyi walimbwende na ninyi wanawake wadogo wanaopendeza wasiwasi: Mtawezaje kustahimili shambulio kuu zaidi la dhoruba? Walimbwende hawajali hata kidogo mazingira wanamojipata. Kwao, linaonekana jambo lisilo la ya maana, wanalipuuza, wao si wabaya, wala hawajioni kuwa hafifu na duni; badala yake wanaendelea kutembea kwa majivuno mitaani wakipeperusha feni zao. Hawa “watu wakubwa” wapumbavu wasiojifunza kamwe hawajui kwa nini Nawaambia mambo kama haya; sura zao zikiwa zimejaa ghadhabu, wao hujaribu tu kujijua, na baadaye wanaendelea na tabia zao ovu; punde wanapotengana nami, wanaaza tena kuwa bila nidhamu duniani, wakifanya hila zao za zamani. Sura yako hubadilika haraka kweli. Kwa hivyo, unajaribu kunidanganya kwa njia hii tena—wewe ni jasiri kweli! Kinachochekesha hata zaidi ni wale wanawake wadogo warembo. Wanaposikia matamshi Yangu ya dharura na kuona mazingira waliomo, machozi yasiyo karibishwa yanatiririka usoni pao, wanajawa na vikweukweu, na wanaonekana kufanya vituko—jambo la kuchukiza kweli! Kwa sababu ya vimo vyao wenyewe, wanajitupa kwenye vitanda vyao na kulala hapo, wakilia bila kukoma, kana kwamba wako karibu kuishiwa na pumzi. Maneno haya yamewaonyesha utoto wao, upuuzi, uhafifu na uduni wao, na baadaye wanalemewa na uhasi, uchangamfu unawaondoka, machoni mwao na, wala kulalamika kunihusu Mimi au kunichukia Mimi, wanakuja kuwa wasiotikisika katikaubaridi wao na vilevile wao wanashindwa kujifunza na wanabaki wajinga. Baada ya kuniacha Mimi, wanafanya mzaha na kuchezecheza, vicheko vyao vinavyovuma vikiwa kama vya “kengele ya Binti wa Kifalme”. Kweli wao ni dhaifu na wasiojipenda! Ninyi nyote, wenye kasoro na kukataliwa ya wanadamu—jinsi gani mnavyokosa ubinadamu! Hamjui jinsi ya kujipenda au jinsi ya kujilinda, hamna akili, hamtafuti njia ya kweli, hampendi mwanga wa kweli na aidha, hamjui jinsi ya kujithamini. Mmeyapuza mafundisho Yangu yaliyorudiwa tangu zamani. Hata mnayachukulia kuwa vitu vya kuchezea wakati hamna shughuli, na daima mnayafikiria kuwa “hirizi yenu wenyewe ya kujilinda.” Mnaposhutumiwa na Shetani, mnaomba; wakati ninyi ni hasi, mnalala; wakati mna furaha, mnakwenda huku na huko; Ninapowashutumu, mnanyenyekea mno; na mnapotengana nami, mnacheka kwa shauku. Ukiwa katika umati, hakuna mwingine mwenye hadhi kubwa kukuliko, lakini kamwe hujioni kuwa fidhuli zaidi kuwaliko wote. Daima wewe ni mwenye kiburi, aliyeridhika na mwenye maringo kukithiri. Je, inawezekanaje “waungwana na wasichana wadogo” na “mabwana na mabibi” ambao hawajifunzi na wanabaki kuwa wajinga wanawezaje kuyachukulia maneno Yangu kuwa hazina ya thamani? Sasa Nitaendelea kukuhoji: Umejifunza nini hasa kutoka kwa maneno na kazi Yangu katika muda mrefu kama huu? Je, hujakuwa mjanja zaidi katika udanganyifu wako? Mstaarabu zaidi katika mwili wako? Wa kawaida zaidi katika

mtazamo wako Kwangu? Nakwambia waziwazi: Nimefanya kazi nyingi sana, lakini imeongeza ujasiri wako, ujasiri ambao awali ulikuwa kama ule wa panya. Hofu yako Kwangu inapunguka kila siku, kwani Mimi ni mkarimu sana, na kamwe sijawatilia vkwazo kwa mwili wako kwa njia ya ukatili; Labda unavyoona, Mimi Nasema maneno makali—lakini kwa mara nyingi huwa Nakutolea tabasamu, na ni nadra ambapo Nakukaripia ana kwa ana. Aidha, Mimi husamehe udhaifu wako kila wakati, na ni kwa sababu ya hili tu ndiyo unanitendea jinsi nyoka humtendea mkulima mzuri. Napendezwa na kiwango chajuu cha ujuzi na ustadi kwa uwezo wa mwanadamu kuchunguza sana! Acha nikwambie ukweli mmoja: Leo haijalishi hata kidogo iwapo una moyo wa uchaji au la; Mimi sina wasiwasi wala wahaka kuhusu hilo. Lakini pia ni lazima Nikuambie hili: Wewe, huyu “mtu mwenye kipaji,” asiyejifunza na anasalia mjinga, hatimaye utaangamizwa na ujanja wako wenye kiburi na kujioenda—ni wewe utakayeteseka na kuadibiwa. Siwezi kuwa mjinga sana kiasi cha kukuandama unapoendelea kuteseka kuzimuni, kwani Mimi silingani na wewe. Usisahau kwamba wewe ni kiumbe aliyelaaniwa na Mimi, na bado aliyefunzwa na kuokolewa na Mimi. Huna chochote Ninachoweza kutotaka kutengana nacho. Kila Nifanyapo kazi, Sizuiliwi na watu, matukio ama vitu vyovyote. Mitazamo na maoni Yangu kuwahusu wanadamu daima yamebaki yale yale. Mimi si mwenye tabia njema kwako hasa, kwa kuwa wewe ni nyongeza kwa usimamizi Wangu na hauko bora sana kuliko kiumbe mwingine. Nakushauri hivi: Kila wakati, kumbuka kwamba wewe ni kiumbe wa Mungu tu! Unaweza kuishi nami, lakini unapaswa kujua utambulisho wako; usijione kuwa wa hadhi ya juu sana. Hata Nisipokushutumu, ama kukushughulikia, na Nakutazama kwa tabasamu, hili halithibitishi kwamba wewe unalingana na Mimi; unapaswa kujua kwamba wewe ni mmoja wa wale wanaofuatilia ukweli, sio ukweli wenyewe! Hupaswi kamwe kukoma kubadili kwa kuambatana na maneno Yangu. Huwezi kuepuka hili. Nakushauri ujaribu kujifunza jambo wakati huu muhimu, fursa hii adimu ikujapo. Usinipumbaze; Sikutaki utumie ubembelezaji kujaribu kunidanganya. Unaponitafuta, yote siyo kwa ajili Yangu, bali kwa ajili yako mwenyewe!

Watu Waliochaguliwa wa China Hawana Uwezo wa Kuwakilisha Kabila Lolote la Israeli

Nyumba ya Daudi ilikuwa ni familia ambayo kiasili ilipokea ahadi na urithi wa Yehova. Ilikuwa kwa asili moja ya makabila ya Israeli na ilikuwa ya watu waliochaguliwa. Wakati huo, Yehova aliamuru sheria iwepo kwa Wana wa Israeli kuwa Wayahudi wote waliokuwa wa nyumba ya Daudi, wale wote waliozaliwa katika nyumba hiyo wangepokea urithi Wake. Wangepokea sehemu mia kwa moja na kupata hadhi ya wana wa kiume wazaliwa wa kwanza. Wakati huo, wao ndio waliokuwa wameinuliwa zaidi miongoni mwa Waisraeli wote—walikuwa na cheo cha juu zaidi miongoni mwa familia zote za Israeli, na walimhudumia Yehova hekaluni

moja kwa moja, kama wamevaa kanzu za ukuhani na mataji. Wakati huo, Yeye aliwaita watumishi waaminifu na watumishi watakatifu nao walipata heshima ya makabila mengine yote ya Israeli. Hivyo, wakati huo wote walitajwa kwa heshima kama mabwana—hii ilikuwa ni kazi ya Yehova katika Enzi ya Sheria. Leo bado wanamhudumia Yehova kwa njia hii katika hekalu, hivyo daima watakuwa wafalme walioteuliwa na Bwana. Hakuna yeyote anayeweza kuwanyang'anya taji lao, na hakuna yeyote anayeweza kubadilisha huduma zao kwa kuwa wao walikuwa ni wa nyumba ya Daudi tangu mwanzo; hili ndilo Yehova amewafadhilia. Sababu ya nyinyi kutokuwa wa nyumba ya Daudi ni kwa sababu nyinyi hamjatoka Israeli, lakini ni mali ya nyumba ya kutoka nje ya Israeli. Kadhalika, asili yenu si kumwabudu Yehova, lakini ni ya kumpinga Yeye, hivyo hamna utambulisho sawa na wa wale wa kutoka nyumba ya Daudi na nyinyi si mojawapo wa wale ambao watapokea urithi Wangu. Nyinyi hasa si wale watakaopokea sehemu mia kwa moja.

Katika Israeli wakati huo kulikuwa na nyumba nyingi tofauti na makabila mengi tofauti, lakini wote walikuwa watu waliochaguliwa. Hata hivyo, kilicho tofauti na nchi zingine ni kwamba katika Israeli watu huanishwa, vyeo vyao mbele ya Yehova vinatofautishwa, na eneo la kila mtu linatandazwa kulingana na makabila yao tofauti. Katika nchi zingine bali na Israeli, hakuna anayeweza kudai kuwa wanyumba za Daudi, Yakobo, au Musa. Hili lingekuwa kinyume cha ukweli—makabila ya Israeli hayawezi kusambazwa pasi na uangalifu katika nchi zingine. Watu mara nyingi hutumia vibaya majina ya Daudi, Ibrahimu, Esau, na kadhalika, au wao husema: “Sisi sasa tumemkubali Mungu, hivyo sisi ni wa nyumba ya Yakobo” Kusema mambo haya si chochote ila kufikiri kwa binadamu kusiko na msingi na mambo haya hayaji moja kwa moja kutoka kwa Yehova, wala kuja kutoka kwa mawazo Yangu Mwenyewe. Ni upuzi wa binadamu tu! Kama mhutubu ambaye husema hadithi ndefu za uongo, bila msingi watu hujifikiria wenyewe kama wa ukoo wa Daudi au sehemu ya familia ya Yakobo, na wanaamini kuwa wao wanastahili hilo. Je, watu hawajui kwamba wale wa nyumba ya Daudi waliamuliwa zamani za kale na Yehova, na hakuwa Daudi aliyejiteua mwenyewe kama mfalme? Hata hivyo, kuna wengi ambao bila haya hudai kuwa wa ukoo wa nyumba ya Daudi—watu ni wajinga sana! Ukweli ni kwamba masuala ya Israeli hayana uhusiano na watu wa mataifa mengine—ni mambo mawili tofauti, na hayahusiani kabisa. Masuala ya Israeli yanaweza tu kuzungumziwa kwa watu wa Israeli, lakini watu wa mataifa hawahusiki kabisa, na kazi inayofanywa sasa miongoni mwa watu wa mataifa haina uhusiano na watu wa Israeli. Kinachosemwa juu watu wa mataifa mengine kinaamuliwa na kile Mimi Ninachokisema sasa, na kazi iliyofanyika Israeli haiwezi kufananishwa na maonyesho ya mbele ya kazi miongoni mwa watu wa mataifa. Je, si hiyo ingeonyesha kwamba Mungu ni wa kawaida sana? Ni wakati tu kazi inapoanza kuenea miongoni mwa watu wa Mataifa ambapo yale yanayosemwa juu yao, au matokeo yake yafichuliwe, ili

maneno ya watu ya siku za nyuma, “Sisi ni wa ukoo wa Daudi,” au “Yesu ni mwana wa Daudi,” ni mambo ya upuuzi hata zaidi kuyasema. Kazi Yangu imetenganishwa. Mimi singemtaja kulungu kama farasi; badala yake, kazi hutofautishwa kulingana na utaratibu wake.

Ufahamu wako wa Baraka ni Upi?

Ingawa wale waliozaliwa katika enzi hii wametiishwa chini ya upotovu wa Shetani na mapepo wachafu sana, pia ni kweli kwamba wanaweza kupata wokovu mkuu kutokana na upotovu huu, hata mkubwa kuliko mifugo wanaotanda milima na tambarare na mali nyingi ya familia ambayo Ayubu alipata, na pia ni zaidi ya baraka ambayo Ayubu alipokea ya kumwona Yehova baada ya majaribu yake. Ilikuwa tu baada ya Ayubu kupitia jaribio la kifo ndipo angeweza kuyasikia maneno ya Yehova na angeweza kusikia sauti Yake ya mshindo kutoka mawinguni. Hata hivyo, hakuuona uso wa Yehova na hakujuua tabia Yake. Kile Ayubu alipata kilikuwa tu mali ya kimwili ambayo hutoa furaha za mwili na watoto wazuri mno katika miji jirani pamoja na ulinzi kutoka kwa malaika wa mbinguni. Hakuwahi kumwona Yehova, na hata ingawa aliitwa mwenye haki, kamwe hakujuua tabia ya Yehova. Ingawa watu wa leo ni maskini kwa muda katika starehe za kimwili au wanapitia mazingira ya nje ya uhasama, Nimedhihirisha tabia Yangu ambayo Sikuwahi kuifunua kwa wanadamu katika vizazi vilivyopita, ambayo siku zote imekuwa siri, na miujiza Yangu kabla ya enzi kwa watu duni mno ambao pia Nimewapa wokovu mkuu, na hii ni mara ya kwanza ambayo Nimefanya hivyo. Sijawahi kufanya aina ya hii awali, na ingawa ninyi mko chini zaidi kuliko Ayubu, yale mmepata na yale mmeona yamemshinda Ayubu kwa mbali. Ingawa mmepitia kila aina ya mateso na maudhi, mateso hayo si kama majaribu ya Ayubu, lakini ni hukumu na kuadibu ambako watu wamepokea kwa sababu ya uasi na ukinzani wao, na kwa sababu ya tabia Yangu yenye haki. Ni hukumu yenye haki, kuadibu, na laana. Ayubu alikuwa mmoja wa Waisraeli, mmoja wa watu wenye haki aliyepokea upendo na rehema ya ajabu ya Yehova. Hakufanya vitendo viovu na hakumpinga Yehova; badala yake, alijitoa kwa Yehova kwa uaminifu, naye alitiishwa chini ya majaribu kwa sababu ya haki yake, na alipitia majaribu makali kwa sababu alikuwa mtumishi mwaminifu wa Yehova. Watu leo wako chini ya hukumu na laana Yangu kwa sababu ya uchafu na uovu wao. Ingawa mateso yao hayalingani kabisa na kile Ayubu alipitia wakati alipoteza mifugo wake, mali yake, watumishi wake, watoto wake, na wale walio wapendwa kwake wote, kile watu wanapitia ni usafishaji na uteketezaji mkali; kilicho kikubwa zaidi kuliko kile Ayubu alipitia ni kwamba aina hii ya jaribio haipunguzwi wala kuondolewa kwa sababu ya udhaifu wao, badala yake, ni ya muda mrefu hadi siku yao ya mwisho ya maisha. Hii ni adhabu, hukumu, laana—ni ya kuteketea bila huruma, na hata zaidi ni “urithi” wa wanadamu wa haki. Ni kile wanachostahili, na ni mahali pa maonyesho ya tabia Yangu yenye haki. Ni ukweli unaojulikana. Lakini yale watu wamepata yanapita sana yale wamevumilia sasa. Yale ambayo mmepitia ni vipingamizi tu

kutokana na upumbavu, lakini mapato yenu ni mara mia zaidi ya mateso yenu. Kwa mujibu wa sheria za Israeli katika Agano la Kale, wale wote wanaonipinga Mimi, wale wote wanaonihukumu waziwazi, na wale wote wasioifuata njia Yangu lakini wanatoa sadaka zenye kukufuru Kwangu kwa ujasiri kwa hakika wataharibiwa kwa moto katika hekalu, au baadhi ya watu waliochaguliwa watawatupia mawe hadi kifo, na hata vizazi vyao vya nyumba yao wenyewe na jamaa zao wengine wa karibu watapitia laana Yangu, na katika dunia ijayo hawatakuwa huru, lakini watakuwa watumwa wa watumwa Wangu, Nami nitawaelekeza hadi uhamishoni miongoni mwa Mataifa nao hawataweza kurudi katika nchi yao. Kulingana na vitendo vyao, tabia zao, mateso yanayovumiliwa na watu leo si makubwa kama adhabu waliyopitia Waisraeli. Kusema kuwa kile mnachopitia sasa ni adhabu si bila sababu, na hii ni kwa sababu mmevuka mpaka kweli, na kama mngekuwa katika Israeli mngekuwa mmoja wa wenye dhambi milele na mngekatwa vipande vipande na Waisraeli muda mrefu uliopita na pia mngeteketezwa kwa moto kutoka mbinguni katika hekalu la Yehova. Na nini ambacho mmepata sasa? Nini ambacho mmepokea, nini ambacho mmefurahia? Nimedhihirisha tabia Yangu yenye haki ndani yenu, lakini muhimu zaidi ni kwamba Nimefunua uvumilivu Wangu kwa ukombozi wa mwanadamu. Mtu angesema kwamba yote ambayo Nimefanya ndani yenu ni kazi na uvumilivu, kwamba ni kwa ajili ya usimamizi Wangu, na hata zaidi ni kwa ajili ya starehe ya wanadamu.

Ingawa Ayubu alipitia majaribu kutoka kwa Yehova, alikuwa tu mtu mwenye haki aliyemwabudu Yehova, na hata alipokuwa akipitia majaribu hayo hakulalamika kumhusu Yeye, lakini alithamini sana kukutana kwake na Yehova. Watu wa leo hawathamini tu uwepo wa Yehova, bali humkataa, humchukia sana, hulalamika kumhusu, na hudhihaki uwepo Wake. Je, hamjapata zaidi ya kidogo? Je, mateso yenu kweli hayajakuwa makubwa sana? Je, baraka zenu hazijakuwa nyingi kuliko zile za Maria na Yakobo? Je, upinzani wenu haujakuwa hafifu? Inawezekana kuwa yale Nimehitaji kwenu, yale Nimeuliza kutoka kwenu yamekuwa makuu mno na mengi sana? Ghadhabu Yangu iliachiliwa huru tu juu ya wale Waisraeli walionipinga Mimi, si moja kwa moja juu yenu, lakini kile ambacho mmepata kimekuwa tu hukumu Yangu isiyo na huruma na mafichuzi pamoja na utakaso mkali usio na huruma. Licha ya haya watu bado wananipinga na kunikana Mimi bila hata chembe ya utii. Na hata kuna baadhi ya watu ambao hujitenga na Mimi na kunikataa; aina hiyo ya mtu si bora zaidi kuliko bendi ya Kora na Dathani wakimpinga Musa. Mioyo ya watu imekuwa migumu sana, na asili zao ni kaidi sana. Kamwe hawatabadili mienendo yao ya zamani. Ninasema wamejiweka wazi kama makahaba hadharani kwa matamshi Yangu, na maneno Yangu ni makali sana kwa kiwango kwamba yanaweza kuwa ya “kukera maskio,” yakiweka wazi asili za watu hadharani—bado wao hukubali tu kwa kutikisa vichwa vyao, wanamwaga machozi machache, na kujilazimisha kuhisi

huzuni kidogo. Mara tu hili linapopita, ni wakali kama mfalme wa wanyama wa pori katika milima na hawana utambuzi kabisa. Je, watu na aina hii ya tabia wanawezaje kujua kwamba wamefurahia baraka zaidi ya mara mia kuliko zile za Ayubu? Wanawezaje kugundua kwamba kile wanachokifurahia ni baraka ambazo zimeonekana katika enzi zote kwa nadra sana, ambazo hakuna mtu aliyewahi kuzifurahia awali? Dhamiri za watu zinawezaje kuhisi aina hii ya baraka ambayo hubeba adhabu? Kusema ukweli, chote Ninachohitaji kwenu ni ili muweze kuwa mifano kwa kazi Yangu na kuwa mashahidi kwa ajili ya tabia Yangu yote na matendo Yangu yote, na ili muweze kuwekwa huru kutokana na mateso ya Shetani. Lakini wanadamu daima huchukizwa na kazi Yangu na wanakuwa na uhasama kwake kimakusudi. Aina hiyo ya mtu anawezaje kutonichochea Mimi kurejesha sheria za Israeli na kuleta juu yake ghadhabu Yangu kwa ajili ya Israeli? Ingawa kuna wengi miongoni mwenu ambao ni “watiifu” Kwangu, kuna hata zaidi ambao wa namna ya “bendi ya Kora” Mara tu Nitakapoupata utukufu Wangu kamili, Nitachukua moto kutoka mbinguni na kuwateketeza hadi wawe majivu. Mnapaswa kujua kwamba Sitawaadibu watu kwa maneno Yangu tena, lakini kabla ya kuifanya kazi ya Israel, Nitaiteketeza kabisa ile namna ya “bendi ya Kora” wanaonipinga Mimi na ambao Nimewaondoa muda mrefu uliopita. Wanadamu hawatapata tena nafasi ya kunifurahia, lakini yote ambayo wataona yatakuwa ghadhabu na “moto” Wangu kutoka mbinguni. Nitaifichua matokeo ya watu wote, na Nitawagawanya watu wote katika makundi mbalimbali. Nitaangalia kila tendo lao lenye uasi, na kisha kuimaliza kazi Yangu, ili matokeo ya watu yataamuliwa kulingana na uamuzi Wangu wakati wako duniani pamoja na mitazamo yao kunihusu. Wakati huo utakapofika, hakutakuwa na kitu kitakachoweza kubadilisha matokeo yao. Acha watu wafunue matokeo yao wenyewe! Acha Niyakabidhi matokeo ya watu kwa Baba wa mbinguni.

Ufahamu Wako Kumhusu Mungu Ni Upi?

Watu wamemwamini Mungu kwa muda mrefu, ilhali wengi wao hawaelewi maana ya neno hili “Mungu”. Wanafuata tu bila kufahamu vyema. Hawajui sababu ya ni kwa nini binadamu anafaa kumwamini Mungu ama Mungu ni nini hasa. Iwapo watu wanajua tu kumfuata na kuamini Mungu, na hawajui Mungu ni nini, wala hawamwelewi Mungu, si huo ni mzaha mkuu ulimwenguni? Ingawa watu wameshuhudia matukio ya kiajabu ya mbinguni wakati huu na wamepata kusikia kuhusu elimu kuu ambayo mwanadamu hajapata kuwa nayo awali, bado wako gizani kuhusu mambo mengi ya kawaida, na ambao ni ukweli ambao haujafikiriwa. Baadhi ya watu wanaweza kusema, “Tumemwamini Mungu kwa miaka mingi. Tutakosaje kujua kufahamu Mungu ni nini? Je, si hili linatudunisha?” Lakini ukweli ni kwamba, ingawa kila mtu ananifuata wakati huu, hakuna yeyote anao ufahamu kuhusu kazi hii yote ya sasa. Hawatili maanani hata maswali ya kawaida na rahisi zaidi, sembuse yale magumu sana kama yanayomhusu Mungu. Mnapaswa kujua kwamba hayo maswali ambayo mnayachukulia kuwa ya kawaida na

hamjayatambua ndiyo mnayopaswa kuyajua zaidi, kwa maana mnajua tu kuufuata umati, hamyatilii maanani wala kuyajali yale ambayo mnafaa kujihami nayo. Je, mnajua kwa uhakika ni kwa nini mnapaswa kuwa na imani kwa Mungu? Je, mnajua kwa uhakika Mungu ni nini? Je, mnajua kwa uhakika binadamu ni nini? Kama mwanadamu ambaye yuko na imani kwa Mungu, iwapo huelewi mambo haya, je, hupotezi hadhi ya mwumini wa Mungu? Kazi Yangu leo ni hii: kuwafanya watu waelewe umuhimu wao, kuelewa yote Ninayoyafanya, na kufahamu uso wa kweli wa Mungu. Hiki ndicho kitendo cha kufunga cha mpango Wangu wa usimamizi, hatua ya mwisho ya kazi Yangu. Ndiyo maana Nawaambia yote kuhusu mafumbo ya maisha mapema, ili nyote muweze kuyakubali kutoka Kwangu. Kwa kuwa hii ndiyo kazi ya nyakati za mwisho, lazima Niwaeleze ukweli wa maisha jinsi ilivyo kwa maana hamjawahi kuyakubali, hata ikiwa huwezi kuyakubali na kuyashika, kwa maana mmepungukiwa sana na hamna matayarisho ya kutosha. Ninataka kumalizia kazi Yangu, kukamilisha kazi yote Ninayopaswa kukamilisha, na kuwafahamisha kikamilifu kuhusu yale Ninayowatuma mfanye, msije mkapotoka tena na kuanguka katika mitego ya mwovu giza linapoingia. Kuna njia nyingi zaidi ya ufahamu wenu, maneno mengi msiyoelewa. Ninyi ni wapumbavu sana. Nazijua hali zenu na upungufu wenu vema. Kwa hivyo, ingawa kuna maneno mengi ambayo hamtaweza kuyaelewa, bado Ninataka kuwaambia ukweli huu wote ambao hamjawahi kuuchukua—kwa kuwa kila mara Ninahofu iwapo, katika hali yenu ya sasa, mtaweza kusimama na kutoa ushuhuda Kwangu. Sio kwamba Nawadhalilisha. Nyote mmekuwa wanyama ambao hawajapitia mafunzo Yangu ya rasmi, na hili ni jambo ambalo linaleta shauku kuhusu kiasi cha utukufu ulio ndani yenu. Ingawa Nimetumia nguvu nyingi kushughulika juu yenu, inaonekana kuwa vipengele vizuri ndani yenu havipo kabisa, ilhali dalili za uovu zinaweza kuhesabika kwa vidole na zinatumika tu kama shuhuda za kumwaibisha Shetani. Takriban kila kitu kingine ndani yenu ni sumu ya Shetani. Mnaonekana Kwangu ni kama ambao mmepita kiwango cha kuokolewa. Kama mambo yalivyo, Naziangalia baadhi ya maonyesho na mienendo yenu, na hatimaye, Najua vimo vyenu halisi. Hiyo ndiyo maana Nina wasiwasi kwa sababu yenu: Akiachwa kuishi maisha peke yake, je, mwanadamu atapata kuwa bora ikilinganishwa na hali ilivyo sasa? Je, hamna wasiwasi kuhusu hali zenu za kitoto? Mnaweza hakika kuwa kama watu wateule wa Uyahudi, kuwa waaminifu Kwangu pekee Yangu katika kila hali? Kile mnachodhihirisha sio mchezo wa watoto ambao wametangatanga kutoka wazazi wao, bali ni unyama unaoonekana katika wanyama ambao wako mbali na mjeledi wa mchungaji wao. Mnapaswa kujua hali yenu halisi, ambayo pia ni udhaifu mlilo nao nyote, ambao ni ugonjwa mlilo nao nyote. Kwa hivyo ombi Langu la pekee kwenu ni kwamba muwe na ushahidi Kwangu. Msije katika hali yoyote kuyaruhusu maradhi ya zamani kuchipuka tena. Jambo la muhimu zaidi ni kutoa ushuhuda. Hicho ndicho kiini cha kazi Yangu. Mnafaa kuyakubali maneno Yangu jinsi Maria alivyokubali ufunuo wa Yehova uliomjia kupitia kwenye ndoto, kuamini na kisha kutii. Hili pekee ndilo linakubalika kama kuwa mtakatifu. Kwa maana

ni ninyi ndio mnasikia neno Langu zaidi, na ambao wamebarikiwa zaidi na Mimi. Ninawapa mali Yangu yote ya thamani, kuwakabidhi kila Nilicho nacho. Hali yenu na ile ya Wayahudi, hata hivyo, ni tofauti kabisa, ni kama nchi mbili tofauti. Lakini mkilinganishwa nao, mnapokea baraka nyingi zaidi yao. Huku wao wakisubiri kwa hamu ili kujitokeza Kwangu, muda mwingi Nimekuwa na ninyi, kutumia utajiri Wangu kwa pamoja. Kwa ulinganisho, ni nini kinachowapa haki ya kunifokea na kuzozana na Mimi na kudai sehemu za mali Yangu? Hampati vya kutosha? Ninawapa vingi sana, lakini Mnachonipa ni huzuni wa kuvunja moyo na dhiki na chuki isiyokomeshwa na kutoridhika. Mnakuwa wazushi sana, ilhali bado mnaiamsha huruma Yangu. Kwa hivyo sina la kufanya ila kuizima chuki Yangu yote na kunena kupinga Kwangu kwenu tena na tena. Katika hii miaka elfu kadhaa ya kazi Yangu, Sikuwa Nimewahi kuleta pingamizi kwa mwanadamu awali kwa kuwa Nilikuwa Nimegundua kwamba katika historia ya kukua kwa mwanadamu, wale waongo zaidi miongoni mweni ndio wanaofahamika zaidi. Wao ni kama urithi wa thamani ambao umeachiwa wewe na “babu” maarufu wa zama za kale. Jinsi gani Ninavyochukia wale nguruwe na mbwa ambao wana upungufu wa ubinadamu. Hamna hisia kabisa! Tabia zenu ni zenye uovu sana! Mioyo yenu ni migumu mno! Iwapo Ningepeleka haya maneno Yangu na hii kazi Yangu kwa Wayahudi, Ninge kuwa nimeshapata utukufu muda mrefu uliopita. Lakini sio hivyo miongoni mweni. Miongoni mweni kuna tu kutojali kwa kikatili, madharau yenu, na visingizio vyenu. Hamna hisia na hamna thamani yoyote kabisa!

Mnafaa kutoa kila kitu chenu kwa ajili ya kazi Yangu. Mnapaswa kufanya kazi inayonifaidi Mimi. Nataka Niwaambie kuhusu yale yote ambayo hamna ufahamu kamili kuyahusu ili muweze kupata yale yote mnayokosa kutoka Kwangu. Hata ingawa kasoro zenu ni nyingi kiasi kwamba haziwezi kuhesabika, Nina nia ya kuendelea kufanya kazi Ninayopaswa kuwa Nikifanya kwenu, kuwapa huruma Zangu za mwisho ili mpate kufaidika kutoka Kwangu, na mpate utukufu ambao hauko ndani yenu na ambao dunia haijawahi kuuona. Nimefanya kazi kwa miaka mingi sana, ilhali hakuna yeyote miongoni mwa binadamu ambaye amewahi kunijua. Nataka kuwaambia siri ambazo sijawahi kumwambia mtu yeyote yule.

Miongoni mwa binadamu, Nilikuwa roho ambaye hawakuweza kuona, Roho ambayo hawangeweza kuigusa. Kwa sababu ya hatua Zangu tatu za kazi duniani (kuumba ulimwengu, ukombozi, na kuiharibu), Naonekana miongoni mwao katika nyakati tofauti (kamwe sio hadharani) ili kutenda kazi Yangu miongoni mwa binadamu. Mara ya kwanza Nilipokuja miongoni mwa binadamu ilikuwa katika Enzi ya Ukombozi. Bila shaka Nilikuja miongoni mwa jamii ya Wayahudi; kwa hivyo watu wa kwanza kumwona Mungu Akija ulimwenguni walikuwa Wayahudi. Sababu Yangu ya kufanya kazi hii mwenyewe ilikuwa kwa sababu Nilitaka kutumia kupata mwili Kwangu kama sadaka ya dhambi katika kazi Yangu ya ukombozi. Kwa hivyo watu wa kwanza kuniona Mimi walikuwa Wayahudi wa Enzi ya Neema. Huo ndio ulikuwa wakati wa

kwanza Mimi kufanya kazi Nikiwa katika mwili. Katika Enzi ya Ufalme, kazi Yangu ni kushinda na kutakasa, kwa hivyo kwa mara nyingine Nafanya kazi ya uchungaji katika mwili. Hii ni mara Yangu ya pili kufanya kazi katika mwili. Katika hatua mbili za mwisho za kazi, wanachokutana nacho watu si tena Roho asiyeonekana, asiyesikika, bali ni mwanadamu ambaye ni Roho Aliyefanyika mwili. Hivyo machoni pa binadamu, Nilikuwa tena mtu asiye na sura wala hisia za Mungu. Zaidi ya hayo, Mungu ambaye watu huona, si wa kiume pekee, bali pia ni wa kike, kitu ambacho ni cha kushtua na kushangaza kwao. Muda baada ya muda, kazi Yangu ya ajabu huziondoa imani za kale ambazo zimekuwa kwa miaka mingi sana. Watu hushangazwa! Huyu Aitwaye Mungu si Roho Mtakatifu pekee, huyo Roho, Roho aliyeongezeka mara saba, Roho anayehusisha yote, bali pia mtu, mtu wa kawaida, mtu wa kipekee wa kawaida. Si wa kiume pekee, bali pia kike. Wako sawa kwamba wote wanazaliwa na binadamu, na tofauti kwamba mmoja alizaliwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na mwingine Anazaliwa kwa mwanadamu lakini Anatoka kwa Roho moja kwa moja. Wako sawa kwa namna kwamba wote kupata miili kwa Mungu hutenda kazi ya Baba yao, na kutofautiana kwa namna kwamba mmoja Anafanya kazi ya ukombozi na mwingine anafanya kazi ya ushindi. Wote wanamwakilisha Mungu Baba, lakini mmoja ni Bwana wa Ukombozi aliyejaa upendo, ukarimu na huruma, na yule mwingine ni Mungu wa uhaki Aliyejaa hasira na hukumu. Mmoja ni Jemadari Mkuu Anayeanzisha kazi ya ukombozi na mwingine ni Mungu wa uhaki wa kukamilisha kazi ya kutamalaki. Mmoja ni Mwanzo na mwingine Mwisho. Mmoja ni mwili usio na dhambi na mwingine ni mwili unaokamilisha ukombozi, Anaendelea na kazi hiyo na kamwe hana dhambi hata. Wote ni Roho mmoja lakini wanaishi katika miili tofauti na walizaliwa katika sehemu tofauti. Na wametenganishwa na maelfu kadhaa ya miaka. Ilhali kazi Zao ni kijalizo kwa nyingine, hazina mgongano kamwe na zinaweza kuzungumziwa kwa wakati mmoja. Wote ni watu, lakini mmoja ni mtoto wa kiume na mwingine mtoto mchanga wa kike. Katika hii miaka yote, ambayo watu wamekiona si Roho pekee na mwanamume, bali pia vitu vingi visivyoambatana na fikira za binadamu, na kwa hivyo hawawezi kunielewa kikamilifu kamwe. Wanashinda wakiniamini mara nyingine na mara nyingine wakiwa na shaka kunihusu, na iwapo Nipo kwa uhakika na ilhali Mimi ni ndoto ya mawazo. Ndio maana mpaka siku ya leo, watu hawatambui Mungu ni nini. Unaweza kweli kunieleza kwa sentensi moja? Unaweza kweli kusema kwa uhakika kwamba “Yesu si mwingine ila ni Mungu, na Mungu si mwingine ila Yesu”? Una ujasiri wa kusema kwamba “Mungu si mwingine bali Roho na Roho si mwingine bali ni Mungu”? Una ujasiri wa kusema kwamba “Mungu ni binadamu tu aliyevalia mwili”? Kwa kweli una ujasiri wa kusema kuwa “Taswira ya Yesu ni taswira kubwa ya Mungu”? Unaweza kuelezea kwa umakinifu tabia ya Mungu na umbo kwa uwezo wa kipawa chako cha maneno? Unaweza hakika kuthubutu kusema kuwa Mungu Aliumba kiume pekee, sio kike, kwa mfano Wake mwenyewe? Ukisema hivi, basi kusingekuwepo na mwanamke miongoni mwa

wateule Wangu na hata zaidi wanawake wasingekuwa aina miongoni mwa wanadamu. Sasa, unajua hakika Mungu ni nini? Je, Mungu ni binadamu? Je, Mungu ni Roho? Je, Mungu kwa uhakika ni wa kiume? Je, ni Yesu pekee Anayeweza kukamilisha kazi ambayo Ninataka kufanya? Ukichagua moja tu kati ya haya kujumuisha kiini Changu, basi utakuwa muumini mjinga kabisa. Nikifanya kazi kama mwili uliopatikana mara moja tu, je, unaweza kuniwekea mipaka? Je, unaweza hakika kuniangalia mara moja na ukajua yaliyo ndani Yangu? Je, unaweza hakika kunieleza kikamilifu kwa mujibu tu wa yale ambayo umeyafahamu wakati wa maisha yako? Na iwapo katika kuingia Kwangu kwa mwili mara mbili Nafanya kazi inayofanana, utanichukulia vipi? Unaweza kuniacha milele msalabani nikiwa na misumari? Je, Mungu anaweza kuwa wa kawaida jinsi unavyosema?

Ijapokuwa imani yenu ni ya kweli kabisa, hakuna kati yenu anayeweza kueleza kunihusu kabisa, na hakuna kati yenu anayeweza kushuhudia uhalisi mnaouona. Tafakari kuhusu jambo hili. Sasa hivi wengi wenu hamyatimizi wajibu wenu, mkifuata vitu vya mwili, mkishibisha mwili na kuburudika kwa mwili. Mnamiliki ukweli mdogo. Mnawezaje basi kushuhudia yote ambayo mmeyaona? Mna uhakika kuwa mtakuwa mashahidi Wangu? Iwapo siku moja utashindwa kushuhudia yote ambayo umeyaona leo, basi utakuwa umepoteza jukumu la kiumbe aliyeumbwa. Hakutakuwa na maana kabisa ya kuwepo kwako. Utakuwa hustahili kuwa binadamu. Mtu anaweza hata kusema kuwa wewe si binadamu! Nimefanya kazi isiyo na kifani kwako. Lakini kwa sababu kwa sasa hujifunzi chochote, hujui chochote, na kufanya kazi bure, Nikitaka kuipanua kazi Yangu utatazama bila kuelewa, bila kusema chochote na kuwa asiye na umuhimu wowote. Hiyo haitakufanya mtenda dhambi mkubwa zaidi? Wakati huo utakapofika, je, hutakuwa na majuto makuu? Hutazama katika huzuni kubwa? Sifanyi kazi hii yote sasa kwa sababu ya kukosa la kufanya na uchoshi, bali kuweka msingi kwa kazi Yangu ya baadaye. Sio kwamba Niko katika njia isiyopitika na Nahitajika kubuni kitu kipya. Unafaa kuelewa kazi ambayo Nafanya; si kitu kinachofanywa na mtoto anayecheza mtaani, bali ni kwa uwakilishi wa Baba Yangu. Unafaa kujua kuwa si Mimi tu Ninayefanya haya yote pekee Yangu bali Namwakilisha Baba Yangu. Wakati uo huo, jukumu lako ni kufuata, kuheshimu, kubadilika, na kushuhudia kwa makini. Unachofaa kuelewa ni kwa nini unafaa kuniamini. Hili ndilo swali muhimu kwa kila mmoja wenu kuelewa. Baba Yangu, kwa ajili ya utukufu Wake, ndiye Aliyewachagua ninyi kwa ajili Yangu kutoka wakati Alipoumba dunia. Haikuwa kwa ajili ya kitu kingine ila kwa ajili ya kazi Yangu na kwa ajili ya utukufu Wake, ndio maana Aliweka hatima yenu awali. Ni kwa sababu ya Baba Yangu ndio unaniamini; ni kwa sababu ya Baba Yangu kukuamua kabla ndio maana unanifuata Mimi. Hakuna kati ya haya ambayo ulichagua kwa hiari yako mwenyewe. La muhimu zaidi ni kwamba muelewe kuwa ninyi ni wale ambao Baba Yangu alinitawazia kwa ajili ya kushuhudia kwa niaba Yangu. Kwa sababu Aliwatawaza

Kwangu, mnafaa kuzifuata njia ambazo Natawaza kwenu na njia na maneno ambayo Ninawafunza, kwani ni jukumu lenu kuzifuata njia Zangu. Hili ndilo kusudi la asili la imani yenu Kwangu. Kwa hivyo Nawaambieni, ninyi ni watu tu ambao Baba Yangu Alitawaza Kwangu ili mfuata njia Zangu. Hata hivyo, mnaamini tu Kwangu; ninyi si wa Kwangu kwa sababu ninyi si wa familia ya Wayahudi bali ni wa joka la zama. Kile Ninachowasihi ni muwe washahidi Wangu, lakini leo lazima mtembee kwa njia Zangu. Haya yote ni kwa ajili ya ushuhuda wa baadaye. Mkihudumu tu kama watu ambao wanasikiliza njia Zangu pekee, basi hamtakuwa na thamani yoyote na umuhimu wa Baba Yangu kuwatawaza Kwangu utapotea. Ninachosisitiza kuwaambia ni hiki: Mnapaswa kutembea katika njia Zangu.

Maana ya Kuwa Mtu Halisi

Kumsimamia mwanadamu ndio Kazi Yangu, na ushindi Wangu dhidi yake ni kitu ambacho kilikuwa hata zaidi kimeshaamuliwa kabla Nilipoiumba dunia. Watu huenda hawajui kwamba Nitashinda kabisa katika siku za mwisho na pia huenda hawajui kwamba ushahidi Wangu kumshinda Shetani ni kuwashinda wale walio waasi miongoni mwa binadamu. Lakini, adui Yangu alipoungana katika vita na Mimi, Nilikuwa Nimeshamwambia kwamba Nitakuwa mshindi wa wale waliokuwa wamechukuliwa na Shetani na kufanywa watoto wake na watumishi wake waaminifu wanaoangalia nyumba yake. Maana ya asili ya kushinda ni kuangamiza, kufedhehesha. Katika lugha Waisraeli walivyoeleza, ni kushinda kabisa, kuharibu, na kumfanya mwanadamu kutoweza kunipinga zaidi. Lakini leo kama linavyotumika kati yenu binadamu, maana yake ni kushinda. Mnapaswa kujua kwamba dhamira Yangu ni kuzima kabisa na kuangamiza yule mwovu kati ya binadamu, ili asiweze tena kuasi dhidi Yangu, sembuse kuwa na pumzi ya kupinga au kuleta fujo kwa Kazi Yangu. Hivyo, kulingana na wanadamu, imekuja kumaanisha kushinda. Haijalishi kidokezo cha neno hili, kazi Yangu ni kumshinda mwanadamu. Kwani, wakati ni ukweli kwamba mwanadamu ni kijalizo cha usimamizi Wangu, kwa usahihi zaidi, mwanadamu si kitu kingine ila ni adui Yangu. Mwanadamu ni yule mwovu anayenipinga na kuniasi. Mwanadamu si mwingine ila kizazi cha yule mwovu aliyelaaniwa na Mimi. Mwanadamu si mwingine ila ukoo wa malaika mkuu ambaye alinisaliti Mimi. Mwanadamu si mwingine ila mrithi wa shetani ambaye, akiwa amekataliwa kwa dharau na Mimi kitambo, amekuwa adui Wangu asiyeweza kupatanishwa tangu wakati huo. Anga iliyo juu ya jamii ya binadamu ni nzito sana, ni yenye giza na huzuni, bila hata dalili ya uwazi, na ulimwengu wa mwanadamu uko katika giza totoro, kiasi kwamba anayeishi ndani yake hawezi hata kuona mkono wake mwenyewe wakati anapounyosha mbele yake au jua anapoinua kichwa chake. Barabara chini ya miguu yake, ni matope na imejaa mashimo makubwa, ni mipindopindo na ya minyongo; nchi yote imejaa maiti. Pembe za giza zimejaa mabaki ya wafu. Na katika pembe zenye baridi na giza magenge ya mapepo yameshika makazi. Na kila mahali katika dunia ya

binadamu, mapepo yanakuja na kwenda katika magenge. Kizazi cha wanyama wa aina yote, waliojawa na uchafu, wanapigana mkono kwa mkono katika mapambano ya kikatili, sauti ambayo huleta hofu moyoni. Nyakati kama hizo, katika dunia kama hiyo, “paradiso ya kidunia” ya aina hii, ni wapi ambako mwanadamu huenda kutafuta bahati ya maisha? Ni wapi ambako mtu ataenda kupata hatima ya maisha yake? Mwanadamu, akiwa amekanyagwa chini ya miguu ya Shetani kwa muda mrefu, amekuwa tangu mwazo mwigizaji akitenda kwa mfano wa Shetani—hata zaidi, kuwa na mwili wake, wakitumika kama shahidi wa kushuhudia kwa Shetani, kwa uwazi. Aina hii ya jamii ya binadamu, aina hii ya watu wachafu walioharibika tabia, na watoto wa aina hii wa familia hii ya binadamu potovu, inawezaje kuwa na ushuhuda kwa Mungu? Utukufu Wangu unatoka wapi? Mtu anaweza kuanza wapi kuongea juu ya shahidi Wangu? Kwa adui ambaye, baada ya kupotosha mwanadamu, anasimama dhidi Yangu, tayari amemchukua mwanadamu—mwanadamu ambaye niliumba kitambo sana na ambaye alikuwa amejawa na utukufu Wangu kuishi kulingana na Mimi—na kumchafua. Amepokonya utukufu Wangu, na yote ambayo imetia moyoni mwa mwanadamu ni sumu iliyojawa na ubaya wa Shetani, na maji ya matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Hapo mwanzo, Nilimuumba mwanadamu, yaani, Nilimuumba babu wa binadamu, Adamu. Alijaliwa na umbo na sura, mwenye kujawa na uhai, kujawa na nguvu ya maisha, na isitoshe, pamoja na utukufu Wangu. Hiyo ilikuwa ni siku tukufu Nilipomuumba mwanadamu. Baada ya hapo, Hawa alitengenezwa kutoka katika mwili wa Adamu, naye alikuwa pia babu wa binadamu, na hivyo watu niliowaumba walikuwa wamejazwa na pumzi Yangu na kujazwa na utukufu Wangu. Adamu kiasili aliumbwa kutoka kwa mkono Wangu na alikuwa akiwasilisha mfano Wangu. Hivyo maana ya asili ya “Adamu” ilikuwa kiumbe kilichoumbwa na Mimi, kilichojawa na nishati Yangu ya uhai, kilichojawa utukufu Wangu, kinacho sura na umbo, kinacho roho na pumzi. Alikuwa kiumbe wa pekee, aliyemilikiwa na roho, ambaye aliweza kuniwakilisha Mimi, kuwa na picha Yangu, na kupokea pumzi Yangu. Hapo mwanzo Hawa alikuwa mtu wa pili kujazwa na pumzi ambaye uumbaji wake nilikuwa nimeamuru, hivyo maana asili ya “Hawa” ilikuwa kiumbe ambaye angeendeleza utukufu Wangu, aliyejazwa na nguvu Zangu na zaidi ya hayo aliyejawa na utukufu Wangu. Hawa aliumbwa kutoka kwa Adamu, kwa hivyo alikuwa pia mfano Wangu, kwa maana yeye alikuwa mtu wa pili kuumbwa kwa mfano Wangu. Maana ya asili ya “Hawa” ilikuwa kiumbe hai, mwenye roho, mwili na mifupa, ushuhuda Wangu wa pili na pia mfano Wangu wa pili miongoni mwa mwanadamu. Walikuwa mababu wa wanadamu, hazina safi na ya thamani ya binadamu, na, kutoka awali, viumbe hai waliojaliwa na roho. Hata hivyo yule mwovu alikichukua kizazi cha mababu wa wanadamu na kukikanyaga na kukiteka nyara, kutosa ulimwengu wa binadamu katika giza totoro, na kuifanya kwamba kizazi chenyewe hakiamini tena katika uwepo Wangu. Kilicho cha chukizo zaidi ni kwamba, hata yule mwovu anapowapotosha watu na kuwakanyagia chini, anapokonya kwa ukatili utukufu Wangu,

ushuhuda Wangu, nguvu Yangu Niliyowatolea watu, pumzi na maisha Niliyopuliza ndani yao, utukufu Wangu wote katika dunia ya binadamu, na damu yote ya roho ambayo nimetumia kwa mwanadamu. Mwanadamu hayupo tena katika mwanga, na amepoteza kila kitu Nilichompa, akiutupilia mbali utukufu ambao nimeutoa. Wanawezaje kukiri kwamba Mimi ndiye Bwana wa viumbe vyote? Wanawezaje kuendelea kuamini kuwepo Kwangu mbinguni? Wanawezaje kugundua udhihirisho wa utukufu Wangu duniani? Hawa wajukuu wa kiume na kike wanaweza kumchukua vipi Mungu ambaye mababu zao walimcha kama Bwana Aliyewaumba? Hawa wajukuu wenye kuhurumiwa “wamewasilisha” kwa ukarimu kwa yule mwovu utukufu, mfano, na vile vile ushahidi ambao Nilikuwa nimewatolea Adamu na Hawa, na pia maisha Niliyompa binadamu na ambayo ategemea ili kuwepo, na, bila kujali hata kidogo uwepo wa yule mwovu, amempa utukufu Wangu wote. Je, si hiki ni chanzo cha jina la “uchafu”? Jinsi gani aina hii ya mwanadamu, mapepo mabaya, aina hii ya maiti inayotembea, aina hii ya umbo la Shetani, na aina hii ya maadui Wangu zinaweza kumilikiwa na utukufu Wangu? Nitaumiliki tena utukufu Wangu, ni umiliki ushuhuda Wangu ambao huwa miongoni mwa wanadamu na vyote vilivyowahi kuwa mali Yangu na Nilivyokuwa Nimewapa wanadamu hapo zamani— nitamshinda mwanadamu kikamilifu. Hata hivyo, unapaswa kujua, wanadamu Nilioumba walikuwa watu watakatifu na wenye mfano Wangu na utukufu Wangu. Hawakuwa wa Shetani, wala hawakukabiliwa na kukanyagwa kwake, bali walikuwa tu udhihirisho Wangu, walikuwa huru kutokana na dalili hata kidogo ya sumu yake. Na hivyo, Niliwajulisha wanadamu wote kwamba Ninataka tu kile kilichoumbwa na mkono Wangu, wale watakatifu ambao nawapenda na wasio wa mwingine yeyote. Aidha, Mimi nitakuwa na furaha nao, na kuwaona kama utukufu Wangu. Hata hivyo, Ninachotaka sio mwanadamu aliyepotoshwa na Shetani, ambaye ni wa Shetani leo, ambaye si kiumbe Changu cha asili tena. Kwa sababu Ninanua kuchukua tena utukufu Wangu katika dunia ya wanadamu, Nitashinda kikamilifu manusura waliobaki kwa wanadamu, kama ushahidi wa utukufu Wangu katika kumshinda Shetani. Mimi huchukua tu ushahidi Wangu kama udhihirisho wa nafsi Yangu, kama kusudi la starehe Yangu. Haya ndiyo mapenzi Yangu.

Mwanadamu ameendelea kwa makumi ya maelfu ya miaka ya historia mpaka kufikia alipo leo. Hata hivyo, mwanadamu wa uumbaji Wangu wa asili kwa muda mrefu uliopita amezama katika upotovu. Tayari amecha kuwa kile Ninachotaka, kwa hivyo wanadamu, Ninavyowaona, hawastahili tena jina la uanadamu. Badala yake wao ni uchafu wa wanadamu, ambao Shetani amewateka nyara, maiti zilizooza zinazotembea ambamo Shetani huishi na huvalia. Watu hawaamini hata kidogo kuwepo Kwangu, wala hawakaribishi kuja Kwangu. Mwanadamu kwa shingo upande tu huyajibu maombi Yangu, na kwa muda anakubaliana nayo, na hashiriki kwa kweli katika furaha na huzuni za maisha pamoja na Mimi. Kwa vile wanadamu huniona Mimi

kama Asiyeeleweka, bila ya kutaka wao hujifanya wanatabasamu Kwangu, kuleta namna ya kujidekeza kwa yule aliye na madaraka. Hii ni kwa sababu watu hawana ufahamu wa kazi Yangu, sembuse mapenzi Yangu kwa wakati wa sasa. Nitakuwa wazi na nyinyi nyote: Siku itakapofika, mateso ya mwanadamu yeyote ambaye huniabudu yatakuwa rahisi kubeba kuliko yenu. Kiwango cha imani yenu Kwangu hakiwezi, kwa hakika, kuzidi kile cha Ayubu—hata imani ya Mafarisayo Wayahudi inaishinda yenu—na hivyo, siku ya moto ikifika, kuteseka kwenu kutakuwa kali zaidi kuliko kule kwa Mafarisayo walipokemewa na Yesu, kuliko kule kwa wale viongozi 250 waliompinga Musa, na kuliko kule kwa Sodoma chini ya moto mkali wa uharibifu wake. Musa alipougonga mwamba, na maji yaliyokuwa yametolewa na Yehova yakaruka, ilikuwa ni kwa sababu ya imani yake. Daudi alipocheza kinubi kwa kunisifu Mimi, Yehova—moyo wake ukiwa umejaa furaha—ilikuwa ni kwa sababu ya imani yake. Ayubu alipowapoteza wanyama wake waliojaa kote milimani na mali nyingi sana, na mwili wake kujawa na majipu mabaya, ilikuwa ni kwa sababu ya imani yake. Alipoweza kusikia sauti Yangu, Yehova, na kuuona utukufu Wangu, Yehova, ilikuwa ni kwa sababu ya imani yake. Kwamba Petro aliweza kumfuata Yesu Kristo, ilikuwa ni kwa imani yake. Kwamba Alitundikwa misumari msalabani kwa ajili Yangu na kutoa ushahidi mtukufu, pia ilikuwa kwa imani yake. Yohana alipoona mfano wa utukufu wa Mwana wa Adamu, ilikuwa kwa imani yake. Alipoona maono ya siku za mwisho, yote yalikuwa zaidi kwa sababu ya imani yake. Sababu ya yanayodaiwa kuwa mataifa mengi yasiyo ya Kiyahudi kupata ufunuo Wangu, na yakajua kwamba Nimerudi katika mwili kufanya kazi Yangu miongoni mwa wanadamu, pia ni kwa sababu ya imani yao. Je si wote ambao wamepigwa na maneno Yangu makali na bado wanafarijiwa nayo na wameokoka—wamefanya hivyo kwa sababu ya imani yao? Wale wanaoamini Kwangu lakini bado hupitia mateso, je si pia wamekataliwa na dunia? Wale wanaoishi nje ya neno Langu, wakikimbia mateso ya majaribu, si wao wote wanazurura tu ulimwengu? Wao ni sawa na majani ya msimu wa kupukutika kwa majani yanayopeperuka hapa na pale, bila pahali pa kupumzika, sembuse neno Langu la kufutia machozi. Ingawa adabu na usafishaji wangu hauwafuati wao, je, wao si waombaji, wanaoelea kila mahali, ambao wakitangatanga katika mitaa iliyo nje ya Ufalme wa mbinguni? Je, dunia ni mahali pako pa mapumziko kweli? Je, unaweza kweli kupata tabasamu hata dhaifu ya kutosheleza kutoka kwa dunia kwa kuepuka adabu yangu? Je, unaweza kweli kutumia starehe zako za kidunia kuficha utupu ulio katika moyo wako usioweza kufichika? Unaweza kumdanganya mtu yeyote katika familia yako, ilhali huwezi kunidanganya Mimi kamwe. Kwa kuwa imani yako ni ndogo sana, mpaka wa leo huna uwezo wa kupata raha inayoletwa na maisha. Nakushauri: heri kutumia nusu ya maisha yako kwa ajili Yangu kwa dhati kuliko kuishi maisha yako yote katika hali hafifu na kujishughulisha kwa ajili ya mwili, kuvumilia mateso yote ambayo ni vigumu binadamu kuvumilia. Kuna faida gani ya wewe kujipenda sana na kuikimbia adabu Yangu? Kuna faida

gani wewe kujificha kutoka kwa adabu Yangu ya muda mfupi tu, na mwishowe kupate aibu ya milele, na adabu ya milele? Mimi, kwa hakika, Simlazimishi yeyote kufanya mapenzi Yangu. Iwapo mtu kweli anayo nia ya kujiwasilisha kwa mipango Yangu yote, Sitamtendea vibaya. Lakini Nahitaji kwamba watu wote waamini ndani Yangu, kama vile Ayubu alivyoamini ndani Yangu, Yehova. Iwapo imani yenu inazidi ile ya Tomaso, basi imani yenu itapata pongezi Zangu, katika uaminifu wenu mtapata furaha Yangu, na hakika mtapata utukufu Wangu katika siku zenu. Hata hivyo, watu, wanaoamini katika dunia na wanaomwamini ibilisi, wamefanya mioyo yao kuwa migumu, kama vile halaiki za mji wa Sodom, na chembe za mchanga zilizovumwa na upepo katika macho yao na sadaka kutoka kwa ibilisi zikiwa zimeshikiliwa vinywani mwao, akili zao zilizodanganywa tangu kitambo zimemilikiwa na yule mwovu ambaye ameipora dunia. Mawazo yao nusura yameporwa na ibilisi wa nyakati za kale. Na hivyo, imani ya mwanadamu imekwenda na upepo, na hawezi hata kuitambua Kazi Yangu. Anachoweza tu kufanya ni kujaribu nkwa unyonge kuvumilia au kuchambua kwa kukisia sana, kwa sababu kwa muda mrefu tayari amejava na sumu ya Shetani.

Mimi Nitawashinda wanadamu kwa sababu wanadanu waliumbwa na Mimi wakati mmoja na pia, kilicho cha ziada, wamefurahia vitu vyote karimu vya uumbaji Wangu. Lakini wanadamu pia wamenikataa Mimi, na nyoyo zao haziko na Mimi ndani yao, na wao huniona kama mzigo kwa uwepe wao, hadi kwa kiwango ambacho, wakiwa kwa kweli wameniona, watu bado wananikataa, na kukuna vichwa wakiwaza kila njia inayoweza kuwawezesha kunishinda Mimi. Watu huwa hawaniruhusu Mimi kuwachukulia kwa umakini au kuweka madai kali juu yao, wala hawanikubali huhukumu au kuadibu udhalimu wao. mbali na kuona hili kuwa jambo la kuvutia, wanakasirika. Na hivyo Kazi Yangu ni kuchukua mwanadamu ambaye hula, hunywa na kusherehekea Kwangu lakini haniujui na kumshinda. Nitawapokonya zana wanadamu, na kisha, Nikiwachukua malaika Wangu, Nikiuchukua utukufu Wangu Nitarejea kwenye makao Yangu. Kwa kuwa kile ambacho watu wamefanya kimenivunja moyo kabisa na kuitawanya kazi Yangu kwa vipande muda mrefu uliopita. Nanuia kuumiliki tena utukufu ambao yule mwovu ameiba kabla ya kuondoka kwa furaha, na kuwaacha wanadamu waendele kuishi maisha yao, waendele na “kuishi na kufanya kazi kwa amani na furaha,” na Mimi sitaingilia kati tena katika maisha yao. Lakini Mimi sasa Nanuia kikamilifu kuumiliki tena utukufu Wangu kutoka kwa mkono wa yule mwovu, kuurejesha ukamilifu wa utukufu Nilioumba ndani ya mwanadamu wakati wa kuumbwa kwa dunia, na kamwe tena kutotolea mwanadamu wa dunia. Kwa kuwa wanadamu hawajashindwa tu kuuhifadhi utukufu Wangu, bali pia wao wameugeuza kuwa mfano wa Shetani. Watu hawathamini kuja Kwangu, wala hawaiwekei thamani siku ya utukufu Wangu. Wao hawasherehekei kupokea adabu Yangu, sembuse kuwa tayari kuurejesha utukufu Wangu Kwangu. Wala hawako tayari kutupa mbali sumu ya yule mwovu. Wanadamu bado siku zote

wananidanganya kwa njia ile ile ya zamani, bado wakivaa tabasamu za kung'aa na nyuso zenye furaha kwa njia ile ile ya zamani. Wao hawajui kina cha huzuni ambayo wanadamu watakabiliwa nao baada ya utukufu Wangu kuwaondoka, na hasa hawajui kwamba siku Yangu itakapokuja kwa wanadamu wote, watakuwa na wakati hata mgumu zaidi kuliko watu katika nyakati za Nuhu. Kwa maana wao hawajui giza iliyokuwepo Israeli wakati utukufu Wangu ulitoweka kwa kuwa mwanadamu husahau kunapokucha jinsi ilivyokuwa vigumu kupita katika giza la usiku wa manane. Jua linaporejea mafichoni tena na giza kumshukia mwanadamu, atanza tena kuomboleza na kusaga meno yake gizani. Je, mmesahau, wakati utukufu Wangu ulipotoweka kutoka Israeli, ilivyokuwa vigumu kwa watu wake kuishi siku zao za mateso? Huu ndio wakati ambapo mnaona utukufu Wangu, na pia ndio wakati ambapo mnashiriki siku ya utukufu Wangu. Mwanadamu ataomboleza katikati ya giza wakati utukufu Wangu unapoondoka kutoka katika nchi chafu. Sasa ndio siku ya utukufu Ninapofanya kazi Yangu, na pia ndio siku ambapo Namwondoa mwanadamu kutoka kwa mateso, kwa kuwa sitapitia nyakati za uchungu na ugumu nao. Mimi Nataka tu ushindi kamili juu ya wanadamu na kumshinda kikamilifu yule mwovu wa wanadamu.

Unajua Nini Kuhusu Imani?

Ndani ya binadamu, kunalo neno lisilokuwa la uhakika, ilhali binadamu hajui imani inajumuisha nini, na vilevile hajui ni kwa nini anayo imani. Binadamu huelewa kidogo sana, na binadamu mwenyewe amepungukiwa sana; yeye anakuwa tu na imani ndani Yangu bila kujali na bila kujua. Ingawa hajui imani ni nini wala ni kwa nini anayo imani ndani Yangu, anaendelea kufanya hivyo kwa shauku mno. Kile Ninachomwomba binadamu, si tu yeye kuniita Mimi kwa shauku kwa njia hii au kuniamini Mimi kwa mtindo huu wa kukosa mwelekeo. Kwani kazi Ninayoifanya ni yake binadamu kunijia Mimi na kunijia Mimi, wala si kwa binadamu kuvutiwa na kuniangalia Mimi kwa njia mpya kwa sababu ya kazi Yangu. Awali Nilijionyesha katika ishara na maajabu mengi na kufanya miujiza mingi. Waisraeli wakati huo waliniangalia Mimi kwa tamanio kuu na walistahi pakubwa uwezo Wangu wa kipekee wa kuponya wagonjwa na kupunga mapepo. Wakati huo, Wayahudi walifikiri nguvu Zangu za uponyaji zilikuwa za kistadi na zisizo za kawaida. Kwa matendo Yangu mengi kama hayo, wote walinichukulia Mimi kwa heshima; waliweza kuhisi tamanio kuu katika nguvu Zangu zote. Kwa hiyo yeyote aliyeniona Mimi nikifanya miujiza alinifuatilia Mimi kwa karibu kiasi kwamba maelfu ya watu walinizunguka ili kunitazama nikiwaponya wagonjwa. Nilionyesha ishara na maajabu mengi, ilhali binadamu alinichukulia Mimi kama daktari stadi; Niliongea maneno mengi ya mafunzo kwa watu hao wakati huo, ilhali wote walinichukulia Mimi tu kama mwalimu aliyekuwa na mamlaka zaidi kwa wanafunzi wake! Hadi siku ya leo, baada ya binadamu kuona rekodi za kihistoria za kazi Yangu, ufasiri wao unaendelea kuwa kwamba Mimi ni daktari mkuu

anayeponya wagonjwa na mwalimu kwa wasiojua. Na wameniiita Mimi Bwana Yesu Kristo Mwenye huruma. Wale wanaofasiri maandiko huenda walizidi mbinu Zangu katika uponyaji, au huenda pengine wakawa wanafunzi ambao tayari wamempita mwalimu wao, ilhali binadamu kama hao wanaofahamika sana ambao majina yao yanajulikana kote ulimwenguni wananichukulia Mimi kwa kiwango cha chini sana cha kuwa daktari tu! Matendo Yangu ni mengi zaidi kwa kuhesabiwa kuliko chembechembe za changarawe kwenye ufuo na hekima Yangu kubwa zaidi kuliko ile ya watoto wote wa kiume wa Suleimani, ilhali binadamu wanafikiria kwamba Mimi ni daktari tu asiye na mengi kumhusu na mwalimu wa binadamu asiyejulikana! Ni wangapi wanaoniamini Mimi ili waweze tu kupata uponyaji? Ni wangapi wanaoniamini Mimi hili tu niweze kutumia nguvu Zangu kupunga roho chafu kutoka kwenye miili yao? Na ni wangapi wanaoniamini Mimi ili tu waweze kupokea amani na furaha kutoka Kwangu? Ni wangapi wanaoniamini Mimi ili kuhitaji kutoka Kwangu utajiri mwingi zaidi wa dunia, na ni wangapi wanaoniamini Mimi ili waweze kuishi maisha hayo kwa usalama na kuwa salama salimini katika maisha yajayo? Ni wangapi wanaoniamini Mimi ili waweze kuepuka tu mateso ya kuzimu na kupokea baraka za mbinguni? Ni wangapi wanaoniamini Mimi ili wapate tulizo lakini hawatafuti kupata chochote kutoka kwa ulimwengu ujao? Niliposhushia hasira Zangu binadamu na kuchukua furaha na amani yote aliyokuwa nayo mwanzo, binadamu akaanza kuwa na shaka. Nilipomkabidhi binadamu mateso ya kuzimu na kuchukua tena baraka za mbinguni, aibu ya binadamu iligeuka na kuwa hasira. Wakati binadamu aliponiomba Mimi kumponya, bado Sikumsikiza na aidha nilimchukia pakubwa, binadamu alienda mbali sana na Mimi na akatafuta njia za dawa ovu na uchawi. Nilipochukua kila kitu ambacho binadamu walitaka kutoka Kwangu, walitoweka bila kuonekana tena. Kwa hivyo, Ninasema kwamba mwanadamu ana imani Kwangu kwa sababu Nampa neema nyingi kupindukia, na mambo yapo mengi sana ya kupata. Wayahudi waliniamini Mimi kwa neema Yangu, na wakanifuata Mimi popote Nilipoenda. Binadamu hawa wasiojua wenye maarifa na uzoefu finyu walitafuta tu kuona ishara na maajabu ambayo nilionyesha. Walinichukulia Mimi kuwa mkuu wa nyumba ya Wayahudi ambaye angeweza kutekeleza miujiza mikubwa zaidi. Kwa hivyo, Nilipopunga mapepo kutoka kwa binadamu walijizungumzia miongoni mwao kwa mkanganyo mkubwa wakisema Mimi ni Eliya, kwamba Mimi ni Musa, kwamba Mimi ndimi nabii wa kale zaidi kati ya wote, kwamba Mimi ndimi daktari mkuu zaidi kuliko wote. Mbali na Mimi Mwenyewe kusema kwamba Mimi ndimi maisha, njia na ukweli, hakuna yeyote angejua uwepo Wangu au utambulisho Wangu. Mbali na Mimi Mwenyewe kusema kwamba mbingu ndipo ambapo Baba Yangu anapoishi, hakuna aliyejua kwamba Mimi ni Mwana wa Mungu, na tena Mungu Mwenyewe. Mbali na Mimi Mwenyewe kusema kwamba Nitaleta ukombozi kwa wanadamu wote na kulipia mwanadamu fidia, hakuna aliyejua Mimi ni Mkombozi wa mwanadamu; binadamu alinijua tu Mimi kama mtu mkarimu na mwenye huruma. Na mbali na Mimi

Mwenyewe kuweza kufafanua kila kitu kuhusu Mimi, hakuna aliyeweza kunitambua Mimi, hakuna aliyeamini kwamba Mimi ni Mwana wa Mungu aliye hai. Binadamu pia anayo imani kama hii Kwangu Mimi, na ananidanganya Mimi kwa njia hii. Binadamu anawezaje kunitolea Mimi ushuhuda wakati anayo mitazamo kama hii kunihusu Mimi?

Binadamu anayo imani Kwangu Mimi lakini hawezi kunitolea ushuhuda Mimi; kabla ya Mimi Mwenyewe kujitambulisha, binadamu hawezi kunitolea ushuhuda Mimi. Binadamu anaona tu kwamba Mimi ninazidi viumbe na binadamu wote wengine watakatifu, na anaona kwamba kazi ninayofanya haiwezi kufanywa na binadamu wengine. Kwa hivyo, kuanzia kwa Wayahudi hadi kwa binadamu wa siku ya leo, yeyote ambaye ameyaona matendo Yangu yenye utukufu anajawa tu na uchu wa kudadisi mengi kuhusu Mimi, ilhali hakuna kinywa cha kiumbe kimoja ambacho kingeweza kunitolea ushuhuda. Baba Yangu tu ndiye Aliyenitolea ushuhuda Mimi; Alinitengenezea njia Mimi miongoni mwa viumbe vyote. Kwani, haijalishi ni namna gani Nilivyofanya kazi, binadamu asingewahi kujua Mimi ndimi Bwana wa viumbe, binadamu anajua tu kuchukua, na hajui kuwa na imani ndani Yangu Mimi kwa sababu ya kazi Yangu Mimi. Binadamu ananijua Mimi tu kwa sababu Mimi sina hatia wala si mtenda dhambi kwa vyovyote vile, kwa sababu Ninaweza kufafanua mafumbo mengi, kwa sababu Mimi niko juu ya wengine wote, au kwa sababu binadamu amefaidi pakubwa kutoka Kwangu. Ilhali wachache ndio wanaoamini kwamba Mimi ndimi Bwana wa viumbe. Hii ndiyo maana Ninasema ya kwamba binadamu hajui ni kwa nini anayo imani Kwangu mimi; hajui kusudio au umuhimu wa kuwa na imani Kwangu mimi. Uhalisia wa binadamu umekosekana, kiasi cha kwamba karibu hana thamani tena ya kuweza kunitolea ushuhuda Mimi. Unayo imani ya kweli ndogo sana na umefaidi kidogo sana, kwa hivyo una ushuhuda mdogo. Aidha, unaelewa mambo machache sana na unapungukiwa na mambo mengi sana kiasi kwamba hufai kushuhudia matendo Yangu. Azimio lako kwa hakika linaeleweka, lakini je una hakika kwamba utaweza kunitolea ushuhuda kwa ufanisi kuhusu hali halisi ya Mungu? Kile ambacho umepitia na kuona kinazidi kile ambacho watakatifu na manabii wengine wa awali walivyoshuhudia, lakini je unaweza kutoa ushuhuda mkubwa zaidi kuliko maneno ya hawa watakatifu na manabii waliotangulia? Kile Ninachokupa wewe sasa kinazidi kile Nilichompa Musa na ni kikubwa zaidi kuliko kile nilichompa Daudi, kwa hivyo vilevile Ninakuomba ushuhuda wako uzidi ule wa Musa na kwamba maneno yako yawe makubwa zaidi kuliko yale ya Daudi. Ninakupa vyote hivi mara mia moja, kwa hivyo vilevile ninakuomba nawe unilipe tena vivyo hivyo. Lazima ujue kwamba Mimi Ndimi ninayempa maisha mwanadamu, na kwamba wewe ndiwe unayepokea maisha kutoka Kwangu na lazima unitolee ushuhuda Mimi. Huu ndio wajibu wako, ambao Ninashusha kwako na ambao unastahili kunifanyia Mimi. Nimekupa utukufu Wangu wote, na kukupatia maisha ambayo watu wateule, Waisraeli, hawakuwahi kupokea. Bila kukosea, unastahili

kunitolea ushuhuda, na kuutoa ujana wako kwa ajili Yangu na kuyatoa maisha yako. Yeyote yule ninayempa Mimi utukufu Wangu ataweza kunitolea Mimi ushuhuda na kunipatia maisha yake. Haya yote yametabiriwa mapema. Ni utajiri wako wewe ambao Ninawekea utukufu Wangu kwako wewe na wajibu wako ni kuutolea ushuhuda utukufu Wangu. Kama unaniamini tu Mimi ili kupata utajiri, basi kazi Yangu haitakuwa yenye umuhimu, na hutakuwa unatimiza wajibu wako. Waisraeli waliona tu huruma Yangu, upendo Wangu na ukubwa Wangu nao Wayahudi walitoa tu ushuhuda wa subira Yangu na ukombozi Wangu. Waliona kazi kidogo sana ya Roho Yangu; huenda ikawa kwamba kiwango chao cha uelewa kilikuwa sehemu ndogo sana ya ile ambayo wewe umesikia na kuona. Kile ulichoona kinazidi hata kile ambacho makuhani wakuu waliona miongoni mwao. Siku hii, ukweli ambao umeelewa umezidi wao; kile ambacho umeona siku hii kinazidi kile kilichoonwa kwenye Enzi ya Sheria pamoja na Enzi ya Neema na kile ambacho umepitia kinazidi hata kile ambacho Musa na Eliya walipitia. Kile ambacho Waisraeli walielewa kilikuwa tu sheria ya Yehova na kile ambacho waliona kilikuwa tu ni mgongo wake Yehova; kile ambacho Wayahudi walielewa kilikuwa tu ukombozi wa Yesu, kile walichopokea kilikuwa neema waliyowekewa na Yesu, na kile walichoona kilikuwa ni taswira ya Yesu ndani ya nyumba ya Wayahudi. Kile utakachoonwa siku hii ni utukufu wa Yehova, ukombozi wa Yesu na matendo Yangu yote ya siku hii. Umesikia pia maneno ya Roho Yangu, hekima Yangu teule, na ukaja kujua kuhusu maajabu Yangu, na umeweza kujifunza kuhusu tabia Yangu. Nimeweza pia kukuambia kuhusu mpango Wangu wa usimamizi. Kile ambacho umeona si tu Mungu mwenye upendo na huruma, lakini yule aliyejawa na haki. Umeiona kazi Yangu ya maajabu na kujua kwamba Nimejawa na hasira na adhama. Aidha, umejua kwamba Niliwahi kuzishusha hasira Zangu katika nyumba ya Israeli, na kwamba leo hii, umeshushiwa wewe. Umeelewa zaidi kuhusu mafumbo Yangu kule mbinguni kuliko vile alivyoelewa Isaya pamoja na Yohana; unajua zaidi kuhusu uzuri Wangu na kustahiwa Kwangu kuliko watakatifu wote wa vizazi vilivyotangulia. Kile ulichopokea si ukweli Wangu tu, njia Yangu, maisha Yangu, lakini maono na ufunuo ambavyo ni vikubwa zaidi kuliko vile vya Yohana. Umeelewa mafumbo mengine mengi zaidi na pia umeona sura Yangu kamili; umekubali mengi kuhusu hukumu Yangu na tabia Yangu ya haki. Kwa hivyo, ingawaje ulizaliwa kwenye siku za mwisho, uelewa wako ni ule wa siku za awali na za kale; umeweza pia kupitia ni nini kilichomo kwenye siku hii, na kile kilichotimizwa na mkono Wangu. Kile Ninachokuomba kinawezekana, kwani kile Nilichokupa ni kingi mno na ni mengi ambayo umeona Kwangu mimi. Kwa hivyo, Ninakuomba kunishuhudia Mimi kama vile watakatifu wa awali walivyofanya na hili ndilo tamanio tu la moyo Wangu.

Ni Baba Yangu ambaye amekuwa akinishuhudia Mimi, lakini Natafuta kupokea utukufu mkubwa zaidi na kwa maneno ya ushuhuda kutoka kwenye vinywa vya viumbe. Kwa hiyo

Ninakupa kila kitu chote Changu kwa kusudi la wewe kuweza kutimiza wajibu wako, kukamilisha kazi Yangu miongoni mwa binadamu. Unastahili kuelewa ni kwa nini una imani Kwangu Mimi. Ukinifuata Mimi tu ili uwe mwanafunzi Wangu au mgonjwa Wangu, au kuwa mojawapo wa watakatifu Wangu mbinguni, basi kunifuata kwako hakutakuwa na maana. Kunifuata Mimi kwa njia kama hiyo ni sawa tu na kuharibu jitihada zako; kuwa na imani kama hiyo Kwangu mimi ni kuishi tu ukiharibu siku zako na kutomakinikia ujana wako. Na mwisho hutapokea chochote. Huku si ni kufanya kazi bure? Ni muda mrefu tangu Nimetoka miongoni mwa Wayahudi na mimi si daktari tena wa binadamu au dawa ya binadamu. Mimi si mnyama tena wa kumbebea mizigo binadamu ili aniendeshe au kunichinja akipenda; badala yake Nimekuja miongoni mwa binadamu ili kuhukumu na kuadibu binadamu, na kwa binadamu kunijua Mimi. Unafaa kujua kwamba Niliwahi kufanya kazi ya ukombozi; Niliwahi kuwa Yesu, lakini Nisingebakia kuwa Yesu milele, licha ya kwamba Niliwahi kuwa Yehova lakini baadaye nikawa Yesu. Mimi ndimi Mungu wa mwanadamu, Bwana wa viumbe, lakini Siwezi kubakia Yesu milele au kubakia Yehova milele. Nimekuwa kile ambacho binadamu aliona ni daktari, lakini haiwezi kusemekana kwamba Mungu ni daktari tu wa mwanadamu. Kwa hiyo kama utakuwa na mtazamo huo wa kale katika imani yako Kwangu mimi, basi hutapata chochote. Haijalishi ni vipi utakavyonisifu siku hii: “Tazama Mungu alivyo na upendo kwa binadamu; Ananiponya mimi na kunipa baraka, amani na furaha. Ni vipi ambavyo Mungu atakavyokuwa mzuri kwa binadamu; kama tutakuwa na imani tu Kwake Yeye, basi hatutahitajika kuwa na wasiwasi wa pesa na utajiri...,” Siwezi bado kutatiza kazi Yangu asilia. Kama utaniamini Mimi siku hii, utapokea tu utukufu Wangu na kustahili kunitolea ushuhuda, na kila kitu kingine kitafuata. Hili lazima ulijue wazi.

Sasa unajua kweli ni kwa nini unaniamini Mimi? Kweli unajua kusudi na umuhimu wa kazi Yangu? Kweli unajua wajibu wako? Kweli unaujua ushuhuda Wangu? Kama unaniamini Mimi tu, ilhali si utukufu Wangu wala ushuhuda Wangu vinaweza kuonekana ndani yako, basi Nimekutupa nje kitambo kirefu. Kwa wale wanaoona wanajua kila kitu, wao ni miiba zaidi katika macho Yangu, na katika nyumba Yangu, wao ni vizuizi tu Kwangu. Wao ndio magugu yanayopaswa kupepetwa kabisa na kuondolewa kwenye kazi Yangu, bila ya jitihada hata kidogo na bila ya uzito wowote; Nimevichukia kitambo kirefu. Na kwa wale bila ya ushuhuda, hasira Yangu siku zote iko juu yao, na kiboko Changu hakijawahi kutoka kwao. Kitambo kirefu Nimewakabidhi kwenye mikono ya yule mwovu, na hawana tena baraka Zangu zozote. Na siku hiyo ikifika, adhabu yao itakuwa mbaya zaidi kuliko ile ya wanawake wajinga. Sasa hivi Ninafanya kazi ile ambayo ndiyo wajibu Wangu kufanya; Nitakusanya pamoja ngano yote, pamoja na magugu. Hii ndiyo kazi Yangu sasa. Magugu haya yataweza kupepetwa na kuondolewa wakati wa kupepetwa Kwangu, kisha nafaka za ngano zitakusanywa kwenye ghala, na

magugu ambayo yatakuwa yamepepetwa yatawekwa motoni na kuchomwa hadi kugeuka jivu. Kazi Yangu sasa ni kuwaweka tu binadamu wote kwa pamoja, yaani, kuweza kuwashinda wote kabisa. Kisha Nitaanza upepetaji wa kufichua mwisho wa binadamu wote. Kwa hiyo unastahili kujua namna ya kunitosheleza Mimi sasa na namna unavyostahili kuwa kwenye njia iliyo sawa katika imani yako Kwangu. Kile Ninachotafuta ni uaminifu na utiifu wako sasa, upendo wako na ushuhuda wako sasa. Hata kama hujui kwa wakati huu kile ambacho ushuhuda unamaanisha au kile ambacho upendo unamaanisha, unafaa kuniletea kila kitu, na kunikabidhi mimi hazina za pekee ulizonazo: uaminifu na utiifu wako. Unafaa kujua, agano la kushinda Kwangu Shetani limo ndani ya uaminifu na utiifu wa binadamu, sawa tu na vile ilivyo katika agano la kumshinda kabisa binadamu. Wajibu wa imani Yako Kwangu mimi ni kunishuhudia Mimi, kuwa mwaminifu Kwangu mimi na si mwingine yeyote, na kuwa mtiifu hadi mwisho. Kabla Sijaanza hatua inayofuata ya kazi Yangu, utawezaje kunishuhudia Mimi? Utawezaje kuwa mwaminifu na mtiifu Kwangu mimi? Je, unajitolea uaminifu wako wote katika utendakazi au utakata tamaa tu? Au afadhali unyenyekee katika kila mpangilio Wangu (uwe wa kifo au wa kuangamiza) au kutoroka hapo katikati ili kuepuka kuadibiwa? Ninakuadibu ili uweze kunishuhudia Mimi, na kuwa mwaminifu na mtiifu Kwangu mimi. Pia, kuadibu huku kwa sasa kunalenga katika kufichua hatua inayofuata ya kazi Yangu na kuruhusu kazi hiyo kuendelea bila kutatizwa. Hivyo basi Nakushawishi wewe kuwa mwenye hekima na kutochukulia maisha yako au umuhimu wa kuwepo kwako kuwa ule ambao hauna manufaa kamwe. Unaweza kujua haswa kazi Yangu ijayo itakuwa ipi? Je, unajua namna Nitakavyofanya kazi katika siku zijazo na namna ambavyo kazi Yangu itakavyobadilika? Unafaa kujua umuhimu wa kile ambacho umepitia katika kazi Yangu, na zaidi, umuhimu wa imani yako Kwangu mimi. Nimefanya mengi kweli; iweje Nikate tamaa Nikiwa katikati kama unavyofikiria? Nimefanya kazi kubwa kweli; ninawezaje kuiharibu? Kwa hakika, Nimekuja kuhitimisha enzi hii. Hii ni kweli, lakini zaidi, lazima ujue kwamba Ninafaa kuanzisha enzi mpya, kuanzisha kazi mpya, na, zaidi ya yote, kueneza injili ya ufalme. Kwa hivyo unafaa kujua kwamba kazi ya sasa inalenga katika kuanzisha tu enzi mpya, na kuweka msingi wa kueneza injili katika wakati ujao na kuihitimisha enzi ya sasa katika wakati ujao. Kazi Yangu si rahisi sana kama unavyofikiria, wala si kwamba haina manufaa au maana kama unavyoweza kutaka kuamini. Kwa hivyo, lazima bado Nikuambie: Unastahili kujitolea maisha Yako katika kazi Yangu, na zaidi, unastahili kujitolea wewe mwenyewe katika utukufu Wangu. Aidha, wewe kunishuhudia ndicho kile kitu ambacho Nimetamani kwa muda mrefu, na kingine ambacho Nimetamani hata zaidi ni wewe kueneza injili Yangu. Unastahili kuelewa kile kilichomo ndani ya moyo Wangu.

**Majani Yaangukayo Yatakaporudi kwa Mizizi Yake, Utajuta
Maovu Yote Ambayo Umefanya**

Nyote mmeshuhudia wenyewe kazi ambayo Nimefanya miongoni mwenu, ninyi wenyewe mmesikia maneno ambayo Nimenena, nanyi mnajua mtazamo Wangu kuelekea kwenu, kwa hiyo mnapaswa kujua kwa nini Ninafanya kazi hii miongoni mwenu. Nitawaambia ukweli—ninyi ni vifaa tu vya kazi Yangu ya ushindi katika siku za mwisho; ninyi ni vyombo vya kupanua kazi Yangu miongoni mwa nchi za Mataifa. Mimi huzungumza kupitia kwa udhalimu wenu, uchafu wenu, upinzani na uasi wenu ili kupanua bora zaidi kazi Yangu ili jina Langu lienee miongoni mwa nchi za Mataifa, yaani, kuenea miongoni mwa nchi yoyote nje ya Israeli. Ni kusudi kwamba jina Langu, vitendo Vyangu, na sauti Yangu viweze kusambaza kotekote katika nchi za Mataifa, hivyo nchi hizo zote ambazo si za Israeli ziweze kushindwa na Mimi na ziweze kuniabudu Mimi, kuwa nchi Zangu takatifu nje ya nchi za Israeli na Misri. Kuipanua kazi Yangu ni kuipanua kwa kweli kazi Yangu ya ushindi, kuipanua nchi Yangu takatifu. Ni kupanua mahali Pangu pa usalama duniani. Mnapaswa kuelewa kwamba ninyi ni viumbe tu miongoni mwa nchi za Mataifa ambazo Mimi huzishinda. Ninyi kwa asili hamkuwa na hali wala thamani yoyote ya kutumia, hakuna matumizi kabisa. Ni kwa sababu tu Niliinua mabuu kutoka kwa rundo la samadi kuwa sampuli za Mimi kuushinda ulimwengu, kuwa “vifaa vya marejeo” pekee vya Mimi kuushinda nchi nzima, ndio mmekuwa na bahati ya kutosha kuwasiliana na Mimi, na kukusanyika na Mimi sasa. Ni kwa sababu ya hadhi yenu ya chini ndiyo Nimewachagua ninyi kuwa sampuli, mifano wa kazi Yangu ya ushindi. Ni kwa sababu hii tu ndiyo Nafanya kazi na kunena miongoni mwenu, na kwamba Naishi na kukaa kwa muda na ninyi. Mnapaswa kujua kwamba ni kwa sababu tu ya usimamizi Wangu na karaha Yangu mno ya ninyi mabuu ndani ya lundo la samadi ndio Nanena miongoni mwenu, na hata ni kwa kiwango cha Mimi kuwa mwenye hasira. Kufanya kazi Kwangu miongoni mwenu sio kabisa sawa na Yehova kufanya kazi katika Israeli, na hasa si sawa na Yesu kufanya kazi Uyahudi. Ni kwa uvumilivu mkuu ndio Nanena na kufanya kazi, na ni kwa hasira na vilevile hukumu ndio Nawashinda wapotovu hawa. Si chochote kama Yehova kuwaongoza watu Wake katika Israeli. Kazi Yake katika Israeli ilikuwa kutoa chakula na maji ya uzima, na Alijawa huruma na upendo kwa watu Wake katika utoaji Wake wa vitu kwao. Kazi ya leo hufanywa katika taifa ambalo halijachaguliwa, ambalo limelaaniwa. Hakuna chakula tele, wala hakuna ustawishaji wa maji ya uzima ya kukata kiu sembuse utoaji wa bidhaa za mwili za kutosha; kunao tu utoaji wa hukumu, laana, na kuadibu vya kutosha. Hawa mabuu katika lundo la samadi hawastahili kwa uthabiti kupata vilima vya ng’ombe na kondoo, utajiri mwingi, na watoto wazuri zaidi kotekote katika nchi ambavyo Nilitoa kwa Israeli. Israeli ya siku hizi hutoa juu ya madhabahu ng’ombe na kondoo na vitu vya dhahabu na fedha ambavyo Mimi huwastawisha navyo, kushinda sehemu moja ya kumi inayotakiwa na Yehova chini ya sheria, na kwa hiyo Nimewapa hata zaidi, zaidi ya mara mia moja ya kile ambacho Israeli ilikuwa ipate chini ya sheria. Kile ambacho Nastawisha Israeli nacho kinashinda kile ambacho Abrahamu na Isaka walipata. Nitaifanya familia ya Israeli kuzaa

na kuongezeka, na Nitawafanya watu Wangu wa Israeli kuenea kutoka upande mmoja hadi upande mwingine wa ulimwengu mzima. Wale ambao Mimi hubariki na kutunza bado ni wateule wa Israeli, yaani, watu ambao hutoa kila kitu Kwangu, ambao wamepata kila kitu kutoka Kwangu. Ni kwa sababu wao huniweka Mimi mawazoni ndiyo wao hutoa sadaka ya ndama na wanakondoo waliozaliwa karibuni juu ya madhabahu Yangu takatifu na hutoa mbele Yangu kila kitu walicho nacho, hata kwa kiwango cha kutoa wana wao wa kwanza waliozaliwa karibuni kwa matarajio ya kurudi Kwangu. Na ninyi je? Ninyi huamsha hasira Yangu, ninyi huwa na matakwa mengi kutoka Kwangu, ninyi huiba sadaka za wale wanaotoa vitu Kwangu na hamjui kwamba mnanikosea Mimi, hivyo mnachopata ni kutoa machozi na adhabu katika giza. Ninyi mmechochea hasira Yangu mara nyingi na Nimenyesha moto Wangu wa kuchoma, kiasi kwamba kumekuwa na wengi waliopatwa na mwisho wa majonzi, ambao makazi yao ya furaha yalikuwa makaburi ya kuhuzunisha. Yote Niliyo nayo kwa mabuu hawa ni hasira isiyoisha, na sina kusudi la baraka. Ni kwa ajili ya kazi Yangu tu ndiyo Nimefanya kinzano na kuwatia ninyi moyo, na kwamba Nimevumilia fedheha kuu kufanya kazi miongoni mwenu. Isingekuwa mapenzi ya Baba Yangu, Ningewezaje kuishi katika nyumba moja na mabuu wanaobingirika kutoka upande mmoja hadi mwingine ndani ya rundo la samadi? Nahisi chuki mno kwa vitendo na maneno yenu yote, na vyovyote vile, kwa sababu Nina “shauku” kiasi katika uchafu na uasi wenu, huu umekuwa mkusanyiko mkubwa wa maneno Yangu. La sivyo Mimi bila shaka singebaki miongoni mwenu kwa muda mrefu hivi. Kwa hiyo, mnapaswa kujua kwamba mtazamo Wangu kuelekea kwenu ni wa upole na huruma tu, mmoja ambao kwao hakuna upendo, ila stahamala tu kwenu, kwa sababu Mimi hufanya hili kwa ajili ya kazi Yangu tu. Na mmeyaona matendo Yangu tu kwa sababu Nimechagua uchafu na uasi kama “mali ghafi.” La sivyo Mimi bila shaka singeyafichua matendo Yangu kwa mabuu hawa; Nafanya tu kazi ndani yenu na usitaji; si chochote kama wepesi na hiari ya kazi Yangu katika Israeli. Nazungumza miongoni mwenu kwa kusita, Nikiibeba hasira Yangu. Isingekuwa kazi Yangu kuu zaidi, Ningewezaje kuvumilia mtazamo wenye kuendelea wa mabuu hawa? Isingekuwa kwa ajili ya jina Langu Ningekuwa Nimepanda vilele vya juu zaidi kitambo na kuwateketeza kabisa hawa mabuu na lundo la samadi! Isingekuwa kwa ajili ya utukufu Wangu, Ningewezaje kuwakubalia pepo hawa waovu kunipinga Mimi waziwazi na vichwa vyao vikitikiswa mbele ya macho Yangu? Isingekuwa kusababisha kazi Yangu kutekelezwa kwa urahisi bila kizuizi hata kidogo, Ningewezaje kuwakubalia hawa watu wanaofanana mabuu kunitusi Mimi kwa utukutu? Kama watu mia moja kijijini mwa Israeli wangeinuka kunipinga Mimi hivi, hata kama wangetoa sadaka Kwangu bado Ningewafutilia mbali chini ya nyufa zilizo ardhini ili watu katika miji mingine hawangeasi tena. Mimi ni moto uteketezao na Sivumilii kosa. Kwa sababu wanadamu wote waliumbwa na Mimi, chochote Nisemacho na kufanya, watu lazima watii na hawawezi kukiasi. Watu hawana haki ya kuingilia kazi Yangu, na wao hasa siyo wenye sifa zinazostahili

kuchambua kilicho cha kweli au chenye makosa katika kazi Yangu na maneno Yangu. Mimi ni Bwana wa uumbaji, na viumbe wanapaswa kutimiza kila kitu Ninachohitaji kwa moyo wa kunicha Mimi; hawapaswi kutoa sababu ili kunishawishi Mimi na wao hasa hawapaswi kunipinga. Ninatumia mamlaka Yangu kuwatawala watu Wangu, na wale wote ambao ni sehemu ya uumbaji Wangu wanapaswa kuyatii mamlaka Yangu. Ingawa leo ninyi ni, jasiri na wenye kiburi mbele Yangu, ninyi hukaidi maneno ambayo Nawafunzia, na hamwogopi, Mimi hukumbana tu na uasi wenu na uvumilivu. Singekasirika na kuathiri kazi Yangu kwa sababu mabuu wadogo sana walipindua uchafu katika rundo la samadi. Mimi huvumilia kuendelea kuwepo kwa kila kitu ambacho Mimi huchukia kabisa na mambo ambayo Mimi huchukia kabisa kwa ajili ya mapenzi ya Baba Yangu, mpaka matamshi Yangu yawe kamili, mpaka dakika Yangu ya mwisho kabisa. Usijali! Siwezi kuzama katika kiwango sawa na buu asiyefaa kutajwa, na Sitafananisha kiwango cha ujuzi na wewe. Nakuchukia kabisa, ilhali Naweza kuvumilia. Wewe hunikaidi Mimi, ilhali huwezi kuepuka siku ya Mimi kukuadibu ambayo Baba Yangu ameniahidi Mimi. Je, buu aliyeumbwa anaweza kufananishwa na Bwana wa uumbaji wote? Katika majira ya kupukutika kwa majani, majani yaangukayo hurudi kwa mizizi yake, wewe hurudi kwa nyumba ya “baba” yako, na Mimi hurudi ubavuni pa Baba Yangu. Mimi huandamana na upendo mwema wa Baba Yangu, na wewe hufuatwa na kuvyogwa kwa baba Yako. Nina utukufu wa Baba Yangu, na wewe una aibu ya baba yako. Mimi hutumia kuadibu ambako Nimeshikilia kwa muda mrefu kuandamana na wewe, na wewe hukutana na kuadibu Kwangu na mwili wako uliooza ambao tayari umekuwa mpotovu kwa makumi ya maelfu ya miaka. Nimehitimisha kazi Yangu ya maneno ndani yako, ikiandamana na uvumilivu, na umeanza kutimiza wajibu wa kupitia msiba kutoka kwa maneno Yangu. Mimi hufurahia sana na kufanya kazi katika Israeli; wewe hulia na kusaga meno yako na huishi na kufa matopeni. Nimepata tena umbo Langu la asili na Sibaki tena ndani ya uchafu na wewe, huku umepata tena ubaya wako wa asili na bado unafukua kila mahali katika lundo la samadi. Wakati ambapo kazi na maneno Yangu yatakamilika, itakuwa siku ya furaha Kwangu. Wakati ambapo upinzani na uasi wako utakwisha, itakuwa siku ya kulia kwako machozi. Sitakuonea huruma, na hutaniona Mimi tena. Sitakuwa tena na mazungumzo na wewe, na hutakutana na Mimi tena. Nitachukia uasi wako, na utakosa kupendeza Kwangu. Nitakupiga wewe, na utanikosa Mimi. Nitaondoka kwako kwa furaha, na utafahamu deni lako Kwangu. Sitakuona wewe tena, lakini wewe kila mara utanitarajia Mimi. Nitakuchukia kwa sababu unanipinga Mimi sasa, na utanikosa Mimi; kwa sababu Nakuadibu sasa. Siko radhi kuishi ubavuni pako, lakini utalitamani sana kwa uchungu na kulia machozi katika milele, kwa sababu utajuta kila kitu ambacho umenifanyia Mimi. Utajuta uasi wako na upinzani wako, na hata utaulaza uso wako juu ya ardhi kutokana na kujuta, na utaanguka chini mbele Yangu na kuapa kutonikaidi Mimi tena. Lakini ndani ya moyo wako wewe hunipenda Mimi tu na hutaweza kamwe kuisikia sauti Yangu, lazima Nikufanye

ujionee haya.

Naona sasa mwili wako usiozuiwa ambao umenibembebeza Mimi, na Nina onyo kidogo tu kwako. Mimi bila shaka sichukui hatua kupitia kuadibu “kukutumikia” wewe. Unapaswa kujua ni wajibu gani ambao wewe huchukua katika kazi Yangu, na kisha Nitaridhika. Kuongezea kwa hili, ukinipinga Mimi au kutumia pesa Zangu, au kula sadaka za Mimi, Yehova, au ninyi mabuu mnaumana, au kuna ugomvi au kuingiliana kati ya ninyi viumbe mfano wa mbwa—Sihusiki na yoyote kati ya hayo. Mnahitaji tu kujua ninyi ni vitu vya aina gani, na Nitaridhika. Mbali na vitu hivi, ni sawa kama mko radhi kuvutiana panga au mikuki au kupigana kwa maneno yenu. Sina tamaa ya kuingilia mambo hayo, na Mimi sihusiki hata kidogo katika mambo ya binadamu. Sio kwamba Sijali kuhusu ugomvi kati yenu, lakini ni kwa sababu Mimi si mmoja wenu, hivyo, Sishiriki katika mambo yaliyo kati yenu. Mimi Mwenyewe si mmoja wa uumbaji na si wa dunia hii, kwa hiyo, Nachukia kabisa maisha ya kuharakisha miongoni mwa watu na hayo mahusiano yasiyofaa, yasiyofaa kati ya watu. Mimi hasa Nachukia kabisa hayo makundi ya makelele ya watu. Hata hivyo, Najua kwa kina uchafu ndani ya mioyo ya kila kiumbe, na kabla ya Mimi kuwaumba ninyi, Nilijua tayari udhalimu uliokuwepo ndani ya kina cha mioyo ya binadamu, na Niliujua udanganyifu na uhalifu wote katika mioyo ya binadamu. Kwa hiyo, hata ingawa hakuna kabisa dalili zozote wakati ambapo watu hufanya mambo ya udhalimu, bado Najua kwamba udhalimu uliowekwa ndani ya mioyo yenu hushinda utajiri wa vitu vyote Nilivyounda. Kila mmoja wenu amepanda vilele vya juu zaidi vya umati; ninyi mmepanda kuwa mababu wa umati. Ninyi ni wadhalimu mno, na mnacharuka miongoni mwa mabuu wote, mkitafuta mahali pa amani na mkijaribu kuwameza mabuu walio wadogo kuwaliko ninyi. Ninyi ni wenye kijicho na wa husuda katika mioyo yenu, kuwashinda wale pepo ambao wamezama chini ya bahari. Mnaishi chini ya samadi, mkiwasumbua mabuu kutoka juu hadi chini ili wasiwe na amani, mkipigana wenyewe kwa wenyewe kwa muda mfupi na kisha kutulia. Ninyi hamjui hali yenu wenyewe, ilhali bado ninyi hupigana wenyewe kwa wenyewe ndani ya samadi. Ni nini ambacho mnaweza kupata kutokana na mapambano hayo? Kama ninyi kweli mngekuwa na moyo wa kunicha Mimi, mngewezaje kupigana wenyewe kwa wenyewe bila Mimi kujua? Haijalishi vile hali yako ilivyo juu, je, bado wewe si mnyoo mdogo mwenye uvundo ndani ya samadi? Utaweza kuota mbawa na kuwa njiwa angani? Ninyi, minyoo wadogo wenye uvundo mnaiba sadaka kutoka kwa madhabahu ya Mimi, Yehova; kwa kufanya hivyo, mnaweza kuokoa majina yenu yaliyoharibika, yenye kasoro kuwa wateule wa Israeli? Ninyi ni mafukara wasio na haya! Hizo sadaka juu ya madhabahu zilizotolewa Kwangu na watu, kuonyesha hisia karimu kutoka kwa wale ambao hunicha Mimi. Ni za udhibiti Wangu na za matumizi Yangu, kwa hiyo inawezekanaje wewe kuniibia Mimi hua wadogo waliotolewa na watu? Je, huogopi kuwa Yuda? Je, huogopi nchi yako kuwa “konde la damu”? Wewe kitu kisicho na haya! Unadhani kwamba

hwa waliotolewa na watu wote ni wa kustawisha tumbo la wewe buu? Kile ambacho Nimekupa ni kile ambacho Nimefurahia na kuwa radhi kukupa wewe; kile ambacho Sijakupa kiko chini ya Mamlaka Yangu, na huwezi tu kuiba sadaka Yangu. Yule Anayefanya kazi ni Mimi, Yehova—Bwana wa uumbaji, na sababu ya watu kutoa sadaka ni Mimi. Unadhani kwamba ni fidia ya kukimbia kila mahali ambako wewe hufanya? Wewe kwa kweli ni usiye haya! Ni nani ambaye unamkimbilia kila mahali? Je, si kwa ajili yako mwenyewe? Kwa nini wewe huiba sadaka Zangu? Kwa nini wewe huiba pesa kutoka kwa mfuko Wangu wa pesa? Je, wewe si mwana wa Yuda Iskariote? Sadaka Zangu, za Yehova, ni za kufurahiwa na makuhani. Je, wewe ni kuhani? Wewe huthubutu kula kwa kujisikia sadaka Zangu na hata unazitandaza juu ya meza; huna thamani yoyote! Wewe fukara asiye na thamani! Moto Wangu, wa Yehova, utakuteketeza wewe!

Hakuna Aliye wa Mwili Anayeweza Kuepuka Siku ya Ghadhabu

Leo, Nawaonya hivi kwa ajili ya kupona kwenu wenyewe, ili kazi Yangu iendele vizuri, na ili kazi Yangu ya uzinduzi kote ulimwenguni iweze kufanyika kwa njia inayofaa na kikamilifu, ikifichua maneno Yangu, mamlaka, adhama na hukumu kwa watu wa nchi zote na mataifa. Kazi Ninayoifanya miongoni mwenu ni mwanzo wa kazi Yangu katika ulimwengu wote. Ingawa sasa ni siku za mwisho tayari, jua kwamba “siku za mwisho” ni jina tu la enzi: Kama tu vile Enzi ya Sheria na Enzi ya Neema, linaashiria enzi, na linaashiria enzi nzima, badala ya mwisho wa miaka au miezi michache. Hata hivyo siku za mwisho ni tofauti kabisa na Enzi ya Neema na Enzi ya Sheria. Kazi ya siku za mwisho haifanyiki katika taifa la Israeli, lakini kati ya mataifa; ni ushindi mbele ya kiti Changu cha enzi cha watu kutoka mataifa yote na makabila yote nje ya Israeli, ili utukufu Wangu katika ulimwengu wote uweze kujaza ulimwengu na anga. Iko hivyo ili Niweze kupata utukufu mkuu, ili viumbe vyote duniani viweze kupitisha utukufu Wangu kwa mataifa yote, milele katika vizazi vyote, na viumbe vyote mbinguni na duniani viweze kuuona utukufu wote ambao Nimepata duniani. Kazi inayofanyika katika siku za mwisho ni kazi ya ushindi. Sio uongozi wa maisha ya watu wote duniani, lakini hitimisho la maisha ya milenia ya mwanadamu yasiyoangamia, ya mateso katika dunia. Matokeo yake ni kwamba kazi ya siku za mwisho haiwezi kuwa kama miaka elfu kadhaa ya kazi katika Israeli, wala haiwezi kuwa kama ile miaka kadhaa tu ya kazi katika Yuda ambayo iliendelea kwa milenia mbili mpaka kupata mwili kwa mara ya pili kwa Mungu katika mwili. Watu wa siku za mwisho hukutana tu na kuonekana tena kwa Mkombozi katika mwili, na kupokea kazi binafsi na maneno ya Mungu. Haitakuwa miaka elfu mbili kabla ya siku za mwisho hazijafika ukingoni; zi fupi, kama wakati ambao Yesu alifanya kazi ya Enzi ya Neema katika Yuda. Hii ni kwa sababu siku za mwisho ni hitimisho la nyakati nzima. Ni ukamilisho na tamatisho la mpango wa miaka elfu sita wa usimamizi wa

Mungu, na kuhitimisha safari ya maisha ya mateso ya mwanadamu. Hazichukui binadamu wote hadi katika enzi mpya au kuruhusu maisha ya mwanadamu kuendelea. Hiyo haitakuwa na umuhimu wowote kwa ajili ya mpango Wangu wa usimamizi au kuwepo kwa mwanadamu. Kama mwanadamu angeendelea kwa namna hii, basi hivi karibuni wao wangeangamizwa kabisa na ibilisi, na zile nafsi za wale walio Wangu hatimaye zingeangamizwa na mikono yake. Kazi Yangu inadumu kwa miaka elfu sita tu, na Mimi niliahidi kwamba udhibiti wa yule mwovu juu ya wanadamu wote utakuwa pia si zaidi ya miaka elfu sita. Na kwa hivyo, wakati umeisha. Nami wala Sitaendelea wala kuchelewa tena: Katika siku za mwisho Nitamshinda Shetani, nami Nitaumiliki tena utukufu Wangu wote, na kurudisha nafsi zile zote zilizo Zangu duniani ili nyoyo hizi za dhiki ziweze kutoroka kutoka bahari ya mateso, na hivyo Nitakuwa nimetimiza kazi Yangu nzima duniani. Kutoka siku hii na kuendelea, kamwe Sitawahi kuwa mwili duniani, na kamwe Roho Wangu wa kudhibiti yote Hatafanya kazi tena duniani. Lakini Nitafanya jambo moja duniani: Nitamfanya tena mwanadamu, mwanadamu aliye mtakatifu, na aliye mji Wangu mwaminifu duniani. Lakini ujue kwamba Sitaiangamiza dunia nzima, wala kuangamiza ubinadamu mzima. Nitahifadhi theluthi moja iliyobaki—theluthi moja inayonipenda na imeshindwa kabisa na Mimi, na Nitaifanya theluthi hii iwe yenye kuzaa matunda na kuongezeka duniani kama Israeli walivyofanya chini ya sheria, kuwalisha kwa kondoo wengi mno na mifugo, na utajiri wote wa dunia. Mwanadamu huyu atabaki na Mimi milele, hata hivyo si mwanadamu mchafu wa kusikitisha wa leo, lakini mwanadamu ambaye ni mkusanyiko wa wale wote ambao wamepatwa na Mimi. Mwanadamu wa aina hii hataharibiwa, kusumbuliwa, au kuzungukwa na Shetani, na atakuwa mwanadamu wa pekee anayepatikana duniani baada ya ushindi Wangu juu ya Shetani. Ni wanadamu ambao leo wameshindwa na Mimi na wamepata ahadi Yangu. Na hivyo, wanadamu ambao wameshindwa katika siku za mwisho pia ndio watakaosamehewa na kupata baraka Zangu za milele. Huu utakuwa ushahidi wa pekee wa ushindi Wangu dhidi ya Shetani, na nyara za pekee za vita Vyangu na Shetani. Hizi nyara za vita zimeokolewa nami kutoka utawala wa Shetani, na ni thibitisho la pekee na matunda ya mpango Wangu wa usimamizi wa miaka elfu sita. Wao huja kutoka kila taifa na dhehebu, na kila mahali na nchi ulimwenguni mwote. Ni wa jamii tofauti, na wana lugha mbalimbali, mila na rangi ya ngozi, na huenea katika kila taifa na dhehebu la duniani, na hata kila pembe ya dunia. Hatimaye, watakuja pamoja na kuunda ubinadamu kamili, mkusanyiko wa binadamu usiofikiwa na majeshi ya Shetani. Wale miongoni mwa wanadamu ambao hawajaokolewa na kushindwa na Mimi watazama kwa kimya mpaka chini ya bahari, na watachomwa kwa moto wa kuteketeza milele. Nitamwangamiza mwanadamu huyu mzee aliye mchafu sana, kama tu vile Nilivyoangamiza wazaliwa wa kwanza na ng'ombe wa Misri, na kuacha tu Waisraeli, waliokula nyama ya mwanakondoo, kunywa damu ya mwanakondoo, na kutia alama vizingitini mwa milango yao kwa damu ya mwanakondoo. Si watu ambao wameshindwa na Mimi na ni wa jamii Yangu ndio

wale pia wanaokula nyama Yangu, Mwanakondoo na kunywa damu Yangu, Mwanakondoo, na wamekombolewa na Mimi na kuniabudu Mimi? Si watu wa namna hiyo kila mara huandamwa na utukufu Wangu? Si hao wasio na nyama Yangu, Mwanakondoo tayari wamezama kimya kwa kina cha bahari? Leo mnanipinga, na leo maneno Yangu ni kama tu yale yaliyosemwa na Yehova kwa wana na wajukuu wa Israeli. Lakini ugumu katika kina cha nyoyo zenu unafanya ghadhabu Yangu kukusanya, na kuleta mateso zaidi juu ya miili yenu, hukumu zaidi juu ya dhambi zenu, na ghadhabu zaidi juu ya udhalimu wenu. Ni nani atakayeweza kusamehewa katika siku Yangu ya ghadhabu, mnaponitendea kwa namna hii leo? Udhalimu wa nani utaweza kuepuka macho Yangu ya kuadibu? Dhambi za nani zinaweza kuepuka mikono Yangu, Mwenyezi? Uasi wa nani unaweza kuhupa hukumu Yangu, Mwenyezi? Mimi, Yehova, Nasema hivyo kwenu, kizazi cha jamii ya Mataifa, na maneno Ninayosema nanyi yanashinda matamko yoyote yale ya Enzi ya Sheria na Enzi ya Neema, ilhali bado nyinyi ni wagumu kuliko watu wote wa Misri. Je, si mnahifadhi ghadhabu Yangu Ninapofanya kazi kwa utulivu? Jinsi gani mnaweza kuepuka salama bila ya madhara kutoka siku Yangu, Mwenyezi?

Nimefanya kazi na kusema kwa njia hii miongoni mwenu, Nimetumia nguvu na juhudi, ila ni wakati upi kamwe mmewahi kusikiliza kile Ninachowaambia wazi wazi? Ni wapi mmeniinamia Mimi, Mwenyezi? Kwa nini mnanitendea namna hii? Kwa nini kila kitu mnachokisema na kufanya huchochea hasira Yangu? Kwa nini, mioyo yenu imeshupaa? Je, Nimewahi kuwapiga kumbo kamwe? Kwa nini hamfanyi kitu chochote kingine ila kunifanya mwenye huzuni na wasiwasi? Mnasubiri siku ya ghadhabu Yangu, Yehova, kuja juu yenu? Je, mnanisubiri Mimi kutuma hasira kwenu iliyochochewa na makosa yenu? Si kila kitu Ninachokifanya ni kwa ajili yenu? Ilhali kila wakati mmenitendea Mimi, Yehova, kwa njia hii: kuiba sadaka Yangu, kuchukua sadaka ya madhabahu Yangu nyumbani kwa jamii ya mbwa mwitu kuwalisha wana wa mbwa mwitu na vitukuu vyake; watu wanapigana wenyewe kwa wenyewe, wakikabiliana na mtazamo wa hasira kwa panga na mikuki, kurusha maneno ya Mimi, Mwenyezi, kwenye choo kuwa machafu kama kinyesi. Uadilifu wenu uko wapi? Ubinadamu wenu umekuwa unyama! Mioyo yenu kwa muda mrefu imegeuka kuwa jiwe. Je, hamjui kwamba siku Yangu ya ghadhabu itakapofika itakuwa ndio wakati Nitakapokuhukumu mabaya mliyotenda dhidi Yangu leo, Mwenyezi? Je, mnafikiri kwamba kwa kunidanganya Mimi kwa njia hii, kwa kutupa maneno Yangu katika matope na kutoyasikiza—unafikiri kwamba kwa kutenda namna hii nyuma Yangu mnaweza kutoroka macho Yangu ya ghadhabu? Je, hamjui kwamba mlishaonekana na macho Yangu, Mimi Yehova, wakati mliiba sadaka Yangu na kutamani mali Yangu? Je, hamjui kwamba wakati mliiba sadaka Yangu, ilikuwa mbele ya madhabahu ambapo dhabihu hutolewa? Mnawezaje kujiamini wenyewe mlivyo wajanja kutosha kunidanganya Mimi kwa njia hii? Ghadhabu Yangu kali ingewezaje kuondoka kutoka katika

dhambi zenu za kuchukiza? Ghadhabu Yangu yenye hasira ingepitaje juu ya matendo yenu maovu? Maovu mnayotenda leo hayawafungulii njia yenu kutokea, bali huhifadhi kuadibu kwa ajili ya kesho yenu; yanachochea kuadibu Kwangu, Mwenyezi, kwenu. Matendo yenu maovu na maneno yenu mabaya yangewezaje kuepuka kuadibu Kwangu? Maombi yenu yangeyafikiaje masikio Yangu? Ningefunguaje njia kwa ajili ya udhalimu wenu? Ningewezaje kuyatupilia mbali matendo yenu maovu ya kunikaidi? Ingewezekanaje Nisizikate ndimi zenu ambazo ni za sumu kama ya nyoka? Hamniombi msaada kwa ajili ya haki yenu, lakini badala yake mnahifadhi ghadhabu Yangu kama matokeo ya udhalimu wenu. Ningewezaje kuwasamehe? Katika macho Yangu, Mwenyezi, maneno na matendo yenu ni machafu. Macho Yangu, Mwenyezi, huona udhalimu wenu kama kuadibu kusikolegea. Kuadibu Kwangu kwa haki na hukumu vingondokaje kwenu? Kwa sababu mmenitendea hivi, na kunifanya mwenye huzuni na ghadhabu, Ningewaachaje nyinyi muepe kutoka mikono Yangu na muondoke katika siku ambayo Mimi, Yehova, Nawaadibu na kuwalaani wewe? Je, hamjui kwamba maneno yenu yote mabaya na matamko tayari yamefikia masikio Yangu? Je, hamjui kwamba udhalimu wenu tayari umelilaghai vazi Langu takatifu la haki? Je, hamjui kwamba makosa yenu tayari yameichochea hasira Yangu kali? Je, hamjui kwamba kwa muda mrefu mmeniacha Nikitokota, na kwa muda mrefu mmeujaribu uvumilivu Wangu? Je, hamjui kwamba tayari mmeshauharibu mwili Wangu kuwa matambara? Nimevumilia mpaka sasa, kiasi kwamba Natoa hasira Zangu, kutokuwa mvumilivu kwenu tena. Je, hamjui kwamba matendo yenu maovu tayari yamefikia Macho Yangu, na kwamba kilio changu tayari kimefikia masikio ya Baba Yangu? Angewaruhusu vipi mnitendee Mimi jinsi hii? Kuna kazi yoyote Ninayofanya ndani yenu isiyo kwa ajili yenu? Ilhali nani kati yenu amekuwa na upendo zaidi kwa kazi Yangu, Yehova? Ningeweza kutokuwa mwaminifu kwa mapenzi ya Baba Yangu kwa sababu Mimi ni mnyonge, na kwa sababu ya uchungu Nilioupitia? Je, hamwelewi Moyo Wangu? Nasema na ninyi kama Yehova alivyofanya; je, Sijajinyima mengi kwa ajili yenu? Hata ingawa Niko tayari kuvumilia mateso haya yote kwa ajili ya kazi ya Baba Yangu, ni jinsi gani nyinyi mnaweza kuachwa huru kutokana na kuadibu ambako Nawaleteni kama matokeo ya mateso Yangu? Je, hamjanifurahia kwa wingi sana? Leo, Nimetolewa kwenu na Baba Yangu; hamfahamu kwamba mnafurahia zaidi ya maneno Yangu mengi? Je, hamjui kwamba maisha Yangu yalibadilishwa na maisha yenu na mambo yote mnayofurahia? Je, hamjui kwamba Baba Yangu alitumia maisha Yangu kupigana na Shetani, na kwamba Yeye pia ametoa maisha Yangu kwenu, na kusababisha nyinyi kupokea mara mia zaidi, na kuwaruhusu kuepuka majaribu mengi? Je, hamjui kwamba ni kwa njia ya Kazi Yangu kwamba mmepewa msamaha kutokana na vishawishi vingi, na kuadibu kwingi kukali? Je, hamjui kwamba ni kwa sababu Yangu tu ndio Baba Yangu anawaruhusu kufurahia mpaka sasa? Jinsi gani mmebaki wagumu na wasiyoyumba leo, kiasi kwamba ni kana kwamba ugume umemea rohoni mwenu? Maovu mnayoyatenda leo yangeepukaje siku ya ghadhabu itakayofuata

kuondoka Kwangu duniani? Ningewezaje kuwaruhusu wale ambao ni wagumu na wasiokubali kuepuka hasira ya Yehova?

Tafakarini kuhusu siku za nyuma: Ni lini macho Yangu yamekuwa na hasira, na sauti Yangu kuwa kali, kwenu? Ni wakati upi Nimegombana nanyi? Ni wakati upi Nimewakaripia bila mantiki? Ni wakati upi Nimewakemea usoni mwenu? Je, si ni kwa ajili ya kazi Yangu ndio kwamba Mimi namwomba Baba Yangu kuwaweka mbali na majaribu? Kwa nini mnanitendea Mimi hivi? Je, Nimewahi kutumia mamlaka Yangu kuipiga miili yenu? Kwa nini mnanilipa Mimi kwa njia hii? Baada ya ninyi kuwa moto na baridi Kwangu, nyinyi si moto wala baridi, na kisha mnajaribu kunirairai Mimi na kuficha mambo kutoka Kwangu, na vinywa vyenu vimejaa mate ya wasio haki. Je, mnafikiri kuwa ndimi zenu zinaweza kumdanganya Roho Wangu? Je, mnafikiri kwamba ndimi zenu zinaweza kuepuka ghadhabu Yangu? Je, mnafikiri kuwa ndimi zenu zinaweza kupitisha hukumu kwa matendo Yangu, Yehova, jinsi zinavyopenda? Je, Mimi ni Mungu ambaye mwanadamu hupishia hukumu? Ningewezaje kuruhusu buu dogo linikufuru hivyo? Ningewezaje kudai wana wa uasi kuwa miongoni mwa baraka Zangu za milele? Maneno na matendo yenu kwa muda mrefu yamewafichua na kuwahukumu. Wakati Nilieneza mbingu na kuumba vitu vyote, Sikuruhusu kiumbe yeyote kushiriki atakavyo, sembuse kuruhusu jambo lolote kuvuruga kazi Yangu na usimamizi Wangu, vile linavyopenda. Sikuvumilia mtu au kitu chochote; Ningewezaje kuwaacha walio wakatili na wa kinyama Kwangu? Ningewezaje kuwasamehe wale ambao wanaasi dhidi ya maneno Yangu? Ningewezaje kuwaacha wanaoniasi? Je, majaliwa ya mwanadamu hayako katika mikono Yangu, Mwenyezi? Ningeuchukua vipi udhalimu wako na uasi kama vitu vitakatifu? Jinsi gani dhambi zako zingenajisi utakatifu Wangu? Mimi sijanajisika na uchafu wa wasio haki, wala kufurahia sadaka ya wasio haki. Kama ungekuwa mwaminifu Kwangu, Yehova, je, ungeweza kujichukulia sadaka kutoka katika madhabahu Yangu? Je, ungeweza kutumia ulimi wako wa sumu kukufuru jina Langu takatifu? Ungeweza kuliasi neno Langu kwa njia hii? Je, ungeweza kuuchukua utukufu Wangu na jina langu takatifu kama chombo ambacho kwalo unamtumikia Shetani, yule mwovu? Maisha Yangu yametolewa kwa ajili ya furaha ya watakatifu. Ningewezaje kukuruhusu ucheze na maisha Yangu jinsi utakavyo, na kuyatumia kama chombo kwa ajili ya migogoro kati yenu? Mngewezaje kuwa wakatili sana, na watovu sana katika njia ya wenye wema, katika jinsi mlivyo Kwangu? Je, hamjui kwamba tayari Nimeandika matendo yenu maovu katika neno hili la maisha? Jinsi gani mngeweza kuepuka siku ya ghadhabu Ninapoadibu Misri? Ningewezaje kuwaruhusu kunipinga na kuniasi kwa njia hii, mara kwa mara? Nawaambia wazi, siku itakapokuja, basi kuadibu kwenu kutakuwa kusikovumilika zaidi kuliko ile ya Misri! Mnawezaje kuitoroka siku ya ghadhabu Yangu? Nawaambia kwa kweli: Uvumilivu Wangu ulitayarishwa kwa ajili ya matendo yenu maovu, na upo kwa ajili ya kuadibu kwenu siku hiyo. Je, ninyi si wale

mtakaopata hukumu ya ghadhabu Yangu punde Nifikapo mwisho wa uvumilivu Wangu? Si mambo yote yapo mikononi Mwangu, Mwenyezi? Ningewezaje kuwaruhusu mniasi hivyo, chini ya mbingu? Maisha yenu yatakuwa magumu sana kwa kuwa mmekutana na Masiha, ambaye ilisemekana Angekuja, lakini ambaye kamwe Hakuja. Je, si nyinyi ni maadui Wake? Yesu amekuwa rafiki wenu, lakini bado mu maadui wa Masiha. Je, hamjui kwamba ingawa nyinyi ni marafiki wa Yesu, matendo yenu maovu yamejaza vyombo vya wale ambao ni wa karaha? Ingawa nyinyi mu karibu sana na Yehova, je, hamjui kwamba maneno yenu mabaya yamefikia masikio ya Yehova na kuchochea ghadhabu Yake? Ingekuwaje awe karibu nawe, na jinsi gani Yeye asingevichoma hivyo vyombo vyako, ambavyo vimejaa matendo mabaya? Ingekuwaje Asiwe adui wako?

Mwokozi Amerudi Tayari Juu ya “Wingu Jeupe”

Kwa maelfu kadhaa ya miaka, mwanadamu ametamani aweze kushuhudia kufika kwa Mwokozi. Mwanadamu ametamani kumtazama Yesu Mwokozi katika wingu jeupe Anaposhuka, yeye binafsi, kati ya wale ambao wamemtamani sana na kumwonea shauku kwa maelfu ya miaka. Mwanadamu ametamani Mwokozi arejee na kuungana na watu, yaani, kwa Yesu Mwokozi kuwarudia watu ambao Amekuwa mbali nao kwa maelfu ya miaka. Na mwanadamu anatumai kuwa Atatekeleza tena kazi ya ukombozi Aliyoifanya kati ya Wayahudi, Atakuwa na huruma na mwenye upendo kwa mwanadamu, Atazisamehe dhambi za mwanadamu, kuchukua dhambi za mwanadamu, na hata kuchukua makosa yote ya mwanadamu na kumkomboa mwanadamu kutoka kwa dhambi. Anatamani Yesu Mwokozi awe jinsi Alivyokuwa hapo awali—Mwokozi ambaye anapendeka, mwema na wa heshima, Asiye na hasira kwa mwanadamu, na Asiyemrudi mwanadamu. Mwokozi huyu Anasamehe na kubeba dhambi zote za mwanadamu, na hata kufa msalabani tena kwa ajili ya mwanadamu. Tangu Yesu aondoke, wafuasi waliomfuata, na watakatifu wote waliookolewa kwa sababu ya jina Lake, wamekuwa wakitamani mno na kumngoja. Wale wote waliookolewa kwa neema ya Yesu Kristo katika Enzi ya Neema wamekuwa wakiitamani siku hiyo ya furaha katika siku za mwisho, wakati ambapo Yesu Mwokozi atawasili juu ya wingu jeupe na kuonekana kati ya mwanadamu. Bila shaka, haya pia ni mapenzi ya pamoja ya wale wote wanaolikubali jina la Yesu Mwokozi leo. Ulimwenguni kote, wale wote wanaojua kuhusu wokovu wa Yesu Mwokozi wamekuwa wakingoja kwa hamu kurejea kwa ghafla kwa Yesu Kristo, ili kutimiza maneno ya Yesu akiwa duniani: “Nitarejea jinsi Nilivyoondoka”. Mwanadamu anaamini kuwa, kufuatia kusulubishwa na kufufuka, Yesu alirudi mbinguni juu ya wingu jeupe, na kuchukua mahali Pake katika mkono wa kuume wa Aliye Juu. Mwanadamu anawaza kuwa vilevile, Yesu atashuka tena juu ya wingu jeupe (wingu hili linarejelea lile wingu ambalo Yesu alipaa juu yake Aliporudi mbinguni), miongoni mwa wale ambao wamemtamani mno kwa maelfu ya miaka, na kwamba Atachukua

mfano na mavazi ya Wayahudi. Baada ya kumwonekana mwanadamu, Atawapa chakula, na kusababisha maji ya uzima kumwagika kwa ajili yao, naye Ataishi miongoni mwa wanadamu, akiwa Amejawa na neema na upendo, Akiwa hai na halisi. Na kadhalika. Ilhali Yesu Mwokozi hakufanya hivi; Alitenda kinyume cha yale ambayo mwanadamu alidhania. Hakurejea kati ya wale ambao walikuwa wametamani kurejea Kwake, naye hakutokea kwa wanadamu wote akiwa Amapanda juu ya wingu jeupe. Amerejea tayari, lakini mwanadamu hamjui, naye anasalia kuwa mjinga kumhusu. Mwanadamu anamngoja tu bila mwelekeo, bila kujua kuwa Ameshuka tayari juu ya “wingu jeupe” (wingu ambalo ni Roho Wake, maneno Yake, na tabia Yake yote na yale yote Aliyo), na sasa yuko kati ya kikundi cha washindi ambacho Atakitengeneza katika siku za mwisho. Mwanadamu hafahamu jambo hili: Ingawa Mwokozi Yesu mtakatifu Amejawa na upendo na mapenzi kwa mwanadamu, Angewezaje kufanya kazi katika “mahekalu” yaliyomilikiwa na uchafu na pepo wachafu? Ingawa mwanadamu amekuwa akingoja kufika Kwake, Angewezaje kuwaonekana wale wanaokula mwili wa wasio na haki, kunywa damu ya wasio na haki, kuvaa mavazi ya wasio na haki, wanaomwamini lakini hawamfahamu, na wanaompokonya kila wakati? Mwanadamu anajua tu kuwa Yesu Mwokozi amejawa na upendo na huruma, naye ni sadaka ya dhambi iliyojawa na ukombozi. Lakini mwanadamu hana habari kwamba Yeye pia ni Mungu Mwenyewe, ambaye Amejawa na haki, uadhama, ghadhabu, na hukumu, na Aliye na mamlaka na kujawa na hadhi. Kwa hiyo ingawa mwanadamu anazamia kwa hamu na kuonea shauku kurudi kwa Mkombozi, na hata Mbingu inaguswa kwa maombi ya mwanadamu, Yesu Mwokozi hawaonekanii wale wanaomwamini ilhali hawamfahamu.

“Yehova” ni jina Nililolichukua wakati wa kazi Yangu kule Uyahudi, nalo linamaanisha Mungu wa Wayahudi (Wateule wa Mungu) Anayeweza kumhurumia mwanadamu, kumlaani mwanadamu, na kuyaongoza maisha ya mwanadamu. Linamaanisha Mungu anayemiliki nguvu kuu na Amejawa na hekima. “Yesu” ni Imanueli, nalo linamaanisha sadaka ya dhambi iliyojawa na upendo, Amejawa na huruma, naye Anamkomboa mwanadamu. Alifanya kazi ya Enzi ya Neema, naye Anawakilisha Enzi ya Neema, na Anaweza tu kuwakilisha sehemu moja ya mpango wa usimamizi. Yaani, Yehova pekee ndiye Mungu wa watu wateule wa Uyahudi, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, Mungu wa Musa, na Mungu wa Wayahudi wote. Na hivyo, katika enzi ya sasa, Waisraeli wote, isipokuwa Wayahudi, wanamwabudu Yehova. Wanamtolea kafara kwa madhabahu, na kumtumikia wakiwa wamevalia mavazi ya kikuhani katika hekalu. Wanachotumainia ni kuonekana tena kwa Yehova. Yesu pekee ndiye Mkombozi wa wanadamu. Yeye ni sadaka ya dhambi ambayo ilimkomboa mwanadamu kutoka kwa dhambi. Yaani, jina la Yesu lilitoka katika Enzi ya Neema, nalo lilikuwepo kwa ajili ya kazi ya wokovu katika Enzi ya Neema. Jina la Yesu lilikuwepo ili kuwawezesha watu wa Enzi ya Neema kuzaliwa upya na kuokolewa, nalo ni jina mahsusi la

wokovu wa binadamu wote. Kwa hiyo jina Yesu linawakilisha kazi ya ukombozi, nalo linaashiria Enzi ya Neema. Jina Yehova ni jina mahsusi la Wayahudi walioishi chini ya sheria. Katika kila enzi na kila hatua ya kazi, jina Langu haliko bila msingi, lakini lina umuhimu wakilishi: Kila jina linawakilisha enzi moja. “Yehova” linawakilisha Enzi ya Sheria, nalo ni jina la heshima kwa Mungu aliyeabudiwa na Wayahudi. “Yesu” linawakilisha Enzi ya Neema, nalo ni jina la Mungu wa wale wote waliokombolewa katika Enzi ya Neema. Iwapo mwanadamu bado anatamani kuwasili kwa Yesu Mwokozi katika siku za mwisho, na bado anamtarajia Afike katika mfano aliochukua kule Uyahudi, basi mpango wote wa usimamizi wa miaka elfu sita ungekoma katika Enzi ya Ukombozi, nao usingeweza kuendelea zaidi. Siku za mwisho, hata zaidi, zisingeweza kufika, nayo enzi isingekomeshwa. Hiyo ni kwa sababu Yesu Mwokozi ni kwa ajili ya ukombozi na wokovu wa wanadamu peke yake. Nililichukua jina la Yesu kwa sababu ya watenda dhambi wote katika Enzi ya Neema, nalo si jina ambalo kwalo Nitawaangamiza wanadamu wote. Ingawa Yehova, Yesu, na Masihi yote yanawakilisha Roho Wangu, majina haya yanaashiria tu enzi tofauti katika mpango Wangu wa usimamizi, nayo hayaniwakilishi katika ukamilifu Wangu. Majina wanayoniita watu duniani hayawezi kueleza kwa ufasaha tabia Yangu nzima na yote Niliyo. Ni majina tofauti tu ambayo Ninaitwa katika enzi tofauti. Na hivyo, enzi ya mwisho—enzi ya siku za mwisho—itakapofika, jina Langu litabadilika tena. Sitaitwa Yehova, au Yesu, wala Masihi, lakini nitaitwa Mwenyezi Mungu Mwenyewe mwenye nguvu, na chini ya jina hili Nitatamatisha enzi nzima. Nilijulikana kama Yehova wakati mmoja. Pia niliitwa Masihi, na wakati mmoja watu waliniita Yesu Mwokozi kwa sababu walinipenda na kuniheshimu. Lakini leo Mimi si yule Yehova au Yesu ambaye watu walimfahamu nyakati zilizopita—Mimi ni Mungu ambaye Amerejea katika siku za mwisho, Mungu ambaye Ataikamilisha enzi. Mimi ni Mungu Mwenyewe ambaye Anainuka kutoka mwisho wa dunia, Nimejawa na tabia Yangu nzima, na Nimejawa na mamlaka, heshima na utukufu. Watu hawajawahi kushirikiana na Mimi, hawajawahi kunifahamu, na daima hawajui tabia Yangu. Tangu uumbaji wa dunia hadi leo, hakuna mtu yeyote ambaye ameniona. Huyu ni Mungu anayemtokea mwanadamu katika siku za mwisho lakini Amejificha kati ya wanadamu. Anaishi kati ya wanadamu, ni wa kweli na halisi, kama jua liwakalo na moto unaochoma, Aliyejaa nguvu na kujawa mamlaka. Hakuna mtu au kitu chochote ambacho hakitahukumiwa kwa maneno Yangu, na mtu au kitu chochote ambacho hakitatakaswa kupitia moto unaowaka. Hatimaye, mataifa yote yatabarikiwa kwa ajili ya maneno Yangu, na pia kupondwa na kuwa vipande vipande kwa sababu ya maneno Yangu. Kwa njia hii, watu wote katika siku za mwisho wataona kuwa Mimi ndiye Mwokozi aliyerejea, Mimi ndiye Mungu Mwenyezi ambaye Anawashinda binadamu wote, nami Nilikuwa sadaka ya dhambi kwa mwanadamu wakati mmoja, lakini katika siku za mwisho Ninakuwa pia miale ya Jua linalochoma vitu vyote, na pia Jua la haki Linalofichua vitu vyote. Hivyo ndivyo ilivyo kazi Yangu ya siku za mwisho.

Nilichukua jina hili nami Ninamiliki tabia hii ili watu wote wapate kuona kuwa Mimi ni Mungu mwenye haki, na Mimi ni jua linachoma, na moto unaowaka. Ni hivyo ili watu wote waweze kuniabudu, Mungu pekee wa kweli, na ili waweze kuuona uso Wangu wa kweli: Mimi si Mungu wa Wayahudi tu, na Mimi si Mkombozi tu—Mimi ni Mungu wa viumbe vyote katika mbingu na dunia na bahari.

Mwokozi atakapofika katika siku za mwisho, kama bado angeitwa Yesu, na kuzaliwa mara nyingine katika Uyahudi, na kufanya kazi Yake katika Uyahudi, basi hii ingethibitisha kuwa Niliumba Wayahudi peke yao na kuwakomboa Wayahudi peke yao, na kuwa Sina uhusiano wowote na Mataifa. Je, hii haitakuwa kinyume cha maneno Yangu kwamba “Mimi ni Bwana aliyeumba mbingu na nchi na vitu vyote”? Nilitoka Uyahudi nami Nafanya kazi Yangu kati ya Mataifa kwa sababu Mimi si Mungu wa Wayahudi tu, ila Mungu wa viumbe vyote. Ninaonekana kati ya Mataifa katika siku za mwisho kwa sababu Mimi si Yehova, Mungu wa Wayahudi tu, lakini, zaidi ya hayo, kwa sababu Mimi ni Muumba wa wateule Wangu wote kati ya Mataifa. Sikuumba Uyahudi, Misri, na Lebanoni pekee, bali pia Niliumba Mataifa yote mbali na Israeli. Na kwa sababu hiyo, Mimi ni Bwana wa viumbe vyote. Nilitumia Uyahudi tu kama hatua ya kwanza ya kazi Yangu, Nikayatumia Uyahudi na Galilaya kama ngome za kazi Yangu ya ukombozi, nami Natumia Mataifa kama msingi ambao Nitatumia kuikamilisha enzi nzima. Nilifanya hatua mbili za kazi katika Uyahudi (hatua mbili za kazi ya Enzi ya Sheria na Enzi ya Neema), nami Nimekuwa Nikitekeleza hatua mbili zaidi za kazi (Enzi ya Neema na Enzi ya Ufalme) katika nchi nyingine zote zaidi ya Uyahudi. Nitafanya kazi ya kushinda kati ya Mataifa, na hivyo kuikamilisha enzi. Mwanadamu akiniita Yesu Kristo kila wakati, lakini hajui kuwa Nimeianza enzi mpya katika siku za mwisho na Nimeanza kazi mpya, na mwanadamu akingoja kwa shauku kuwasili kwa Yesu Mwokozi, basi Nitawaita watu kama hao wale wasioniamini. Wao ni watu ambao hawanijui, na imani yao Kwangu ni ya bandia. Je, watu kama hao wanaweza kushuhudia kufika kwa Yesu Mwokozi kutoka mbinguni? Wanachongoja si kufika Kwangu, bali ni kufika kwa Mfalme wa Wayahudi. Hawatamani maangamizo Yangu ya dunia hii nzee yenye uchafu, lakini badala yake wanatamani kurudi kwa Yesu kwa mara ya pili, ndipo watakapokombolewa; wanamtazamia Yesu kuwakomboa wanadamu wote mara nyingine kutoka nchi hii iliyochafuliwa na isiyo na haki. Watu kama hao watawezaje kuwa wale wanaoikamilisha kazi Yangu katika siku za mwisho? Matamania ya mwanadamu hayawezi kufikia mapenzi Yangu ama kutimiza kazi Yangu, kwani mwanadamu hutamani au kuthamini tu kazi ambayo Nimeifanya hapo awali, naye hajui kuwa Mimi ni Mungu Mwenyewe ambaye ni mpya siku zote na si mzee kamwe. Mwanadamu anajua tu kuwa Mimi ni Yehova, na Yesu, naye hana fununu kuwa Mimi ni Mwisho, Yule ambaye Atawaangamiza wanadamu. Mwanadamu anachotamani na kujua tu ni kuhusu dhana yake mwenyewe, nayo ni yale tu ambayo anaweza kuyaona kwa macho

yake mwenyewe. Hayako sambamba na kazi Ninayoifanya, bali hayatangamani nayo. Kama kazi Yangu ingefanywa kulingana na mawazo ya mwanadamu, basi ingeisha lini? Mwanadamu angeingia katika pumziko lini? Nami Ningewezaje kuingia katika siku ya saba, Sabato? Nafanya kazi kulingana na mpango Wangu, kulingana na lengo Langu, na sio kulingana na nia ya mwanadamu.

Kazi ya Kueneza Injili Ni Kazi ya Kuokoa Binadamu Pia

Watu wote wanahitaji kuelewa kusudio la kazi Yangu ulimwenguni, yaani, lengo la mwisho la kazi Yangu na ni kiwango kipi ambacho lazima Nitimize katika kazi hii kabla inaweza kukamilika. Kama, baada ya kutembea na Mimi hadi leo, watu hawaelewi kazi Yangu inahusu nini, basi hawajakuwa wakitembea na Mimi bure? Watu wanaonifuata Mimi wanafaa kujua mapenzi Yangu. Nimekuwa nikifanya kazi ulimwenguni kwa maelfu ya miaka, na hadi leo ningali nafanya kazi Yangu vivyo hivyo sasa. Ingawa kunavyo vipengele vingi hasa vilivyojumuishwa katika kazi Yangu, kusudio la kazi hii linabakia lilelile. Kwa mfano, ingawa Nimejazwa na hukumu na adabu kwa binadamu, kila ninachofanya bado ni kwa ajili ya kumwokoa binadamu, kwa ajili ya kueneza injili Yangu kwa njia bora zaidi na kupanua zaidi kazi Yangu miongoni mwa Mataifa baada ya binadamu kufanywa kuwa kamili. Kwa hiyo leo, katika wakati ambapo watu wengi tayari wametamauka pakubwa, Naendelea na kazi Yangu, Nikiendeleza kazi ambayo lazima Nifanye ili kuhukumu na kuadibu binadamu. Licha ya ukweli kwamba binadamu amechoshwa na kile Ninachosema na licha ya ukweli kwamba hana tamanio la kujali kuhusu kazi Yangu, Ningali natekeleza wajibu Wangu kwa sababu kusudio la kazi Yangu halijabadilika na mpango Wangu asilia hautabadilika. Kazi ya hukumu Yangu ni kumfanya binadamu anitii Mimi kwa njia bora zaidi, na kazi ya kuadibu Kwangu ni kuruhusu binadamu awe na mabadiliko bora zaidi. Ingawa kile Ninachofanya ni kwa minajili ya usimamizi Wangu, Sijawahi kufanya chochote ambacho hakikufaidi binadamu. Hiyo ndiyo maana Nataka kufanya mataifa yote nje ya Israeli yawe na utii kama tu Waisraeli na kuwabadilisha kuwa binadamu halisi, ili Niwe na mahali pa usalama katika nchi zilizo nje ya Israeli. Huu ndio usimamizi Wangu; ndiyo kazi Ninayotimiza katika nchi za Mataifa. Hata sasa, watu wengi bado hawaelewi usimamizi Wangu kwa sababu hawajautilia maanani, badala yake wanafikiria tu kuhusu mustakabali na hatima zao. Haijalishi ni nini Ninachosema, watu hawajali kazi Yangu, badala yake wanalenga tu hatima zao za baadaye. Mambo yakiendelea kwa namna hii, kazi Yangu itapanuliwa vipi? Injili Yangu itaenezwa vipi kotekote ulimwenguni? Lazima mjue kwamba wakati kazi Yangu inapanuka, Nitawatawanya, Nitawaadhibu kama vile tu Yehova alivyoyaadhibu makabila ya Israeli. Haya yote yatafanywa ili injili Yangu iweze kuenea kotekote kwenye ulimwengu mzima, ili kazi Yangu iweze kuenezwa kwa Mataifa, ili kwamba jina Langu litukuzwe na watu wazima na watoto kwa pamoja na jina Langu takatifu litatukuzwa katika

vinywa vya watu kutoka makabila na mataifa yote. Ili kwamba katika enzi hii ya mwisho jina Langu litatukuzwa miongoni mwa Mataifa, kwamba matendo Yangu yataonekana na mataifa mengine na wataniita Mwenyezi kwa sababu ya matendo Yangu, na kwamba maneno Yangu yatatimika karibuni. Nitawafanya watu wote wajue kwamba Mimi siye tu Mungu wa Waisraeli, lakini Mimi ni Mungu wa Mataifa yote, hata mataifa yale Niliyoyalaani. Nitawafanya watu wote waone kwamba Mimi ndimi Mungu wa viumbe vyote. Hii ndiyo kazi Yangu kubwa zaidi, kusudio la mpango wa kazi Yangu katika siku za mwisho, na kazi ya pekee kutimizwa katika siku za mwisho.

Kazi ambayo Nimekuwa nikisimamia kwa maelfu ya miaka inafichuliwa kabisa tu kwa binadamu katika siku za mwisho. Ni sasa tu ndipo Nimelifumbua fumbo kamili la usimamizi Wangu kwa mwanadamu. Binadamu anajua kusudio la kazi Yangu na zaidi ya yote anapata uelewa wa mafumbo Yangu yote. Na Nimemwambia binadamu kila kitu kuhusu hatima ambayo amekuwa akijali kuhusu. Tayari Nimemfichulia binadamu mafumbo yote yaliyofichwa kwa zaidi ya miaka 5,900. Yehova ni nani? Masiha ni nani? Yesu ni nani? Mnafaa kuyajua haya yote. Mabadiliko makubwa ya kazi Yangu yamo katika majina haya. Je, mmelewa haya? Jina Langu takatifu linafaa kutangazwa vipi? Jina Langu linafaa kuenezwaje katika taifa lolote ambalo limeniita kwa jina Langu lolote? Kazi Yangu tayari imeanza kupanuka, na Nitaeneza ukamilifu wake katika mataifa yote. Kwa sababu kazi Yangu imetekelezwa ndani yenu, Nitawapiga kama vile Yehova alivyowapiga wale wachungaji wa nyumba ya Daudi kule Israeli, na kuwasababisha kutawanyika miongoni mwa mataifa yote. Kwani katika siku za mwisho, Nitapondaponda mataifa yote kuwa vipande vidogo vidogo na kusababisha watu wao kuenezwa upya. Nitakaporudi tena, mataifa yatakuwa tayari yamegawanywa kwa mipaka iliyowekwa na mwako wa moto Wangu utakaokuwa ukichoma. Katika wakati huo, Nitajionyesha upya kwa binadamu kama jua linalochoma, Nikijionyesha kwao hadharani kwa taswira ya yule Aliye Mtakatifu ambaye hawajawahi kumwona, Nikitembea miongoni mwa mataifa yote, kama vile tu Mimi, Yehova, Nilivyotembea miongoni mwa makabila ya Wayahudi. Kuanzia hapo kuendelea, Nitawaongoza watu huku wakiishi ulimwenguni. Hakika wataona utukufu Wangu hapo na hakika wataona pia nguzo ya wingu hewani ili uwaongoze, kwani Nitaonekana katika sehemu takatifu. Binadamu ataiona siku Yangu ya haki na pia maonyesho Yangu ya utukufu. Hilo litafanyika Nitakapoutawala ulimwengu mzima na kuwaleta wana wengi katika utukufu. Kila pahali duniani, watu watainama, nalo hema Langu takatifu litaundwa miongoni mwao juu ya mwamba wa kazi ambayo Natekeleza sasa. Watu watanihudumia pia hekaluni. Madhabahu, yaliyojaa mambo machafu na ya kuchukiza, Nitayavunjavunja vipandevipande na Nitajenga upya mengine. Madhabahu matakatifu yatarundikwa wanakondoo na ndama waliozaliwa karibuni. Nitaangusha hekalu lililopo leo na kujenga jingine upya. Hekalu lililopo sasa na

lililojaa watu wenye chuki litaporomoka na lile Nitakalojenga litajaa watumishi watiifu Kwangu. Kwa mara nyingine watasimama na kunihudumia Mimi kwa utukufu wa hekalu Langu. Kwa hakika mtaiona siku ambayo Nitapokea utukufu mkuu na hakika mtaiona siku ambayo Nitaliangusha hekalu na kujenga lingine upya. Pia, hakika mtaona siku ya kuletwa kwa hema Langu takatifu hapa ulimwenguni mwa binadamu. Huku Nikilibomoa hekalu, ndivyo Nitakavyoleta hema Langu takatifu hapa ulimwenguni mwa binadamu; itakuwa kama vile tu ambavyo watu wanavyoniona Nikishuka. Baada ya kuangamiza mataifa yote, Nitayakusanya pamoja upya, Nikilijenga hekalu Langu na kuandaa madhabahu Yangu, ili wote waweze kutoa kafara zao Kwangu, kunihudumia Mimi hapo, na kujitolea kwa uaminifu katika kazi Yangu kwenye mataifa mengineyo. Itafanywa namna tu ambavyo wana wa Israeli wanavyofanya sasa, na joho la kuhani na taji la mfalme, utukufu Wangu, Yehova, ukiwa miongoni mwao na uadhama Wangu ukivinjari juu yao na ukiwa nao. Kazi Yangu katika Mataifa itatekelezwa pia katika njia hiyo. Kama vile kazi Yangu kule Israeli ilivyokuwa, ndivyo kazi Yangu katika Mataifa itakavyokuwa kwa sababu Nitaongeza kazi Yangu kule Israeli na kuieneza katika mataifa yale mengine.

Sasa ndio wakati ambao Roho Wangu anafanya kazi pakubwa, na wakati Ninapofanya kazi miongoni mwa Mataifa. Hata zaidi, ndio wakati ambapo Naainisha viumbe wote na kuweka kila kiumbe katika kundi lenye uhusiano, ili kazi Yangu iweze kuendelea haraka zaidi na kwa njia ya kufaa zaidi. Kwa hiyo, bado Nahitaji kwamba mjitoe mzimamzima kwa minajili ya kazi Yangu yote; aidha, mnafaa kutambua waziwazi na kuwa na hakika ya kazi ile yote ambayo Nimefanya ndani yako, na kuweka nguvu zako zote katika kazi Yangu ili iweze kuwa ya matokeo bora zaidi. Hilo ndilo ambalo lazima uelewe. Msipigane tena wenyewe kwa wenyewe, kutafuta mbinu za usuluhishi, au kutafuta raha za mwili, mambo ambayo yanaweza kuchelewesha kazi Yangu na kuharibu mustakabali wako mzuri. Kufanya hivyo, mbali na kuweza kukupa ulinzi, litakuletea maangamizo. Je, si huu utakuwa ujinga kwa upande wako? Kile ambacho unafurahia leo kwa tamaa ndicho kile kile ambacho kinaharibu mustakabali wako, huku yale maumivu unayopitia leo ndiyo yaleyale ambayo yanakulinda. Lazima ufahamu waziwazi kuhusu jambo hilo, ili uepuke majaribio ambayo yatakuwa magumu kujinasua kutoka na kuepuka kuingia kwenye ukungu mzito unaozuia jua katika maisha yako. Wakati ukungu huu mzito utakapotoweka, utajipata katika hukumu ya siku kuu. Kufikia wakati huo, siku Yangu itakuwa imekaribia binadamu. Utatorokaje hukumu Yangu? Utawezaje kuvumilia joto kali la jua? Ninapompa binadamu wingi Wangu, haufurahii kwa dhati, lakini badala yake anautupa nje kwenye sehemu zisizotambulika. Wakati siku Yangu itawadia, binadamu hataweza tena kugundua wingi Wangu au kupata ukweli mkali Niliompa zamani sana. Ataomboleza na kulia, kwa sababu amepoteza mwangaza anaofuata na kuingia katika giza totoro. Kile mnachoona leo ni upanga tu mkali wa

kinywa Changu. Bado hamjakiona kiboko kilicho katika mkono Wangu au moto Ninaotumia kumchoma binadamu, na ndiyo maana bado mna kiburi na msio na kadiri mbele Yangu. Ndiyo maana bado mnapigana na Mimi katika nyumba Yangu, huku mkipinga kwa ulimi wa mwanadamu kile ambacho Nimenena na kinywa Changu. Binadamu haniogopi Mimi. Akiwa bado katika uhasama na Mimi hadi leo, bado haniogopi kamwe. Mnao ulimi na meno ya wale wasio na haki vinywani mwenu. Maneno na matendo yenu ni kama yale ya yule nyoka aliyemshawishi Hawa na kumfanya kutenda dhambi. Mnadai nyinyi kwa nyinyi kulipiza kisasi, na mnashindana mbele Yangu kwa ajili ya nafasi, umaarufu, na faida kwa ajili yenu wenyewe, ilhali hamjui kwamba Natazama maneno na matendo yenu kwa siri. Kabla hata ya nyinyi kuja mbele Yangu, Nimejua vina vya nyoyo zenu kabisa. Siku zote binadamu hutamani kutoroka kutoka mfumbato Wangu na kuepuka uangalizi wa macho Yangu, lakini Sijawahi kuepuka maneno au matamshi yake. Badala yake, kwa kusudio kuu huwa Nayaruhusu maneno na matendo hayo yaingie katika macho Yangu, ili Niweze kuadibu udhalimu wake na kuhukumu uasi wake. Kwa hiyo, maneno na matendo fiche ya binadamu siku zote yanawekwa mbele ya kiti Changu cha hukumu, na hukumu Yangu haijawahi kumtoka binadamu, kwa sababu uasi wake ni mwingi mno. Kazi Yangu ni kuteketeza na kusafisha maneno na matendo yote ya binadamu yaliyotamkwa na kufanywa mbele ya Roho Wangu. Kwa njia hiyo, baada ya Mimi kuondoka ulimwenguni, binadamu wataweza bado kuendeleza utiifu Kwangu, na bado watanihudumia kama vile watumishi Wangu watakatifu wanavyofanya katika kazi Yangu, wakiruhusu kazi Yangu hapa ulimwenguni iendele mpaka siku itakapokamilika.

Ninyi Nyote Ni Waovu Sana Katika Tabia!

Ninyi nyote huketi kwenye viti vya umbuji, mkiwakaripia wale wa vizazi vidogo ambao ni wa namna yenu na mkiwafanya waketi pamoja nanyi. Ila hamjui kwamba “wazawa” wenu waliishiwa na pumzi kitambo sana na kuipoteza kazi Yangu. Utukufu Wangu unang’aa kutoka katika nchi ya Mashariki hadi katika nchi ya Magharibi, lakini utakapoenea hadi miisho ya dunia na kuanza kuinuka na kuangaza, Nitauchukua utukufu Wangu kutoka Mashariki na kuuleta Magharibi ili kwamba watu waovu, ambao wamenitelekeza huko Mashariki watanyimwa mwangaza kuanzia wakati huo na kuendelea. Hilo litakapofanyika, mtaishi katika bonde la kivuli. Hata ingawa watu siku hizi ni bora mara mia moja kuliko hapo awali, bado hawawezi kutimiza matakwa Yangu, na bado wao sio ushuhuda kwa utukufu Wangu. Kwamba mnaweza kuwa bora mara mia moja kuliko hapo awali ni matokeo ya kazi Yangu kabisa; ni matunda yatokanayo na kazi Yangu duniani. Hata hivyo, bado Ninahisi kuchukizwa na maneno na matendo yenu, na vile vile na tabia yenu, na Ninahisi chuki kubwa sana kuhusu jinsi mnavyotenda mbele Yangu, kwa kuwa hamna ufahamu wowote kunihusu. Basi, mnawezaje kuja kuishi kwa kudhihirisha utukufu Wangu, na mnawezaje kuwa waaminifu kabisa kwa kazi Yangu

ya baadaye? Imani yenu ni ya kupendeza sana; mnasema kwamba mko tayari kutumia maisha yenu yote kwa ajili ya kazi Yangu, na kwamba mko tayari kutoa maisha yenu kwa ajili ya kazi hiyo, lakini tabia zenu hazijabadilika sana. Mnazungumza tu kwa kiburi, licha ya ukweli kwamba tabia yenu halisi ni mbovu sana. Ni kana kwamba ndimi na midomo ya watu iko mbinguni lakini miguu yao iko chini duniani, na kwa sababu hiyo, maneno na matendo yao na sifa zao bado ni mbovu na zisizoheshimika. Sifa zenu zimeharibiwa, tabia yenu imepotoka, njia yenu ya kuzungumza ni duni, na maisha yenu ni yenye kustahili dharau; hata ubinadamu wenu wote umezama katika hali duni ya chini kabisa. Ninyi ni wenye mawazo finyu kuhusu wengine, na ninyi hubishana kuhusu kila jambo dogo. Ninyi hugombana kuhusu heshima na hadhi zenu wenyewe, hadi kufikia kiwango ambapo mko tayari kushuka kuzimuni na kuingia kwenye ziwa la moto. Maneno na matendo yenu ya sasa yanatosha Mimi kubaini kwamba ninyi ni wenye dhambi. Mitazamo yenu kwa kazi Yangu inatosha Mimi kubaini kuwa ninyi ni wadhalimu, na tabia zenu zote zinatosha kuonyesha kwamba ninyi ni watu wachafu mliojaa machukizo. Maonyesho yenu na kile mnachofichua vinatosha kusema kwamba ninyi ni watu ambao mmekunywa damu ya roho wachafu hadi mkatosheka. Kuingia katika ufalme kunapotajwa, hamfichui hisia zenu. Je, mnaamini ya kwamba jinsi mlivyo sasa inatosha kwa ninyi kupita katika lango la kuingia katika ufalme Wangu wa mbinguni? Je, mnaamini ya kwamba mnaweza kuingia katika nchi takatifu ya kazi na maneno Yangu, bila maneno na matendo yenu wenyewe kujaribiwa na Mimi kwanza? Ni nani anayeweza kunihadaa? Tabia na mazungumzo yenu yenye kustahili dharau na yaliyo duni yanaweza kuepukaje macho Yangu? Maisha yenu yamebainiwa na Mimi kuwa maisha ya kunywa damu na kula nyama ya roho hao wachafu kwa sababu ninyi huwaiga mbele Yangu kila siku. Mbele Yangu, tabia yenu imekuwa mbaya hasa, kwa hiyo Ninawezaje kukosa kuwaona kuwa wenye kuchukiza? Maneno yenu yana uchafu wa roho wachafu: Mnabembeleza, kuficha na kujipendekeza kama tu wale wanaoshiriki katika uchawi na kama wale walio wadanganyifu na wanaokunywa damu ya wadhalimu. Maonyesho yote ya mwanadamu ni dhalimu mno, kwa hivyo watu wote wanaweza kuwekwaje katika nchi takatifu ambako wenye haki wako? Je, unafikiri kwamba hiyo tabia yako yenye kustahili dharau inaweza kukubainisha kama mtakatifu ikilinganishwa na wale wadhalimu? Ulimi wako ulio kama wa nyoka hatimaye utauangamiza huu mwili wako ambao huleta uharibifu na kutekeleza machukizo, na hiyo mikono yako iliyojaa damu ya roho wachafu pia hatimaye itaipeleka roho yako jahannamu. Basi, kwa nini huipokei kwa furaha nyingi fursa hii ili uitakase mikono yako iliyojaa uchafu? Na kwa nini huchukui fursa hii kwa manufaa yako uukate huo ulimi wako unaozungumza maneno ya kudhulumu? Je, inawezekana kwamba uko tayari kuteseka katika moto wa jahannamu kwa ajili ya mikono, ulimi na midomo yako? Mimi huuchunga moyo wa kila mtu kwa macho yote mawili, kwa sababu muda mrefu kabla Niwaumbe wanadamu, Nilikuwa nimeifumbata mioyo yao mikononi Mwangu. Nilikuwa nimeibaini mioyo ya watu

kitambo, kwa hiyo mawazo yao yangeyaepukaje macho Yangu? Muda utakosaje kuwa umewaishia wa kuepuka kuchomwa na Roho Wangu?

Midomo yako ni mikarimu zaidi kuliko njiwa, lakini moyo wako ni mwovu zaidi kuliko yule nyoka wa zamani. Midomo yako ni ya kupendeza hata kama wanawake wa Lebanoni, lakini moyo wako si mwema zaidi kuliko yao, na hakika hauwezi kulinganishwa na uzuri wa Wakanaani. Moyo wako ni mdanganyifu mno! Vitu Ninavyochukia ni midomo na mioyo ya wadhalimu tu, na matakwa Yangu kwa watu si ya juu zaidi ya yale Ninayotarajia kutoka kwa watakatifu hata kidogo; ni kwamba tu Natiwa kinyaa kwa ajili ya matendo maovu ya wadhalimu, nami Natumai kwamba waweze kutupilia mbali uchafu wao na kutoroka kutoka katika hatari waliyomo sasa ili waweze kusimama kutoka kwa hao wadhalimu na wawe watakatifu na kuishi na wale ambao ni wenye haki. Ninyi mko katika hali sawa na Yangu, lakini mmejaa uchafu; hamna hata mfano kidogo zaidi wa asili wa wanadamu walioumbwa hapo mwanzo. Aidha, kwa sababu kila siku mnaiiga mifano ya hao roho wachafu, mkifanya kile wanachofanya na kusema kile wanachosema, kila sehemu yenu—hata ndimi na midomo yenu—imeloweza katika maji yao machafu, kiasi kwamba mmejaa madoa kama hayo kabisa, na hakuna sehemu yenu hata moja inayoweza kutumika kwa ajili ya kazi Yangu. Ni jambo la kusikitisha sana! Mnaishi katika dunia ya farasi na ng’ombe kabisa, lakini kwa kweli hamhisi kufadhaishwa; mmejaa furaha na mnaishi kwa uhuru na bila matatizo. Mnaogelea huku na kule katika maji hayo machafu, lakini kwa kweli hamtambui ya kwamba mmeingia katika hatari kama hiyo. Kila siku, mnaandamana na roho wachafu na kuingiliana na “kinyesi.” Maisha yenu ni ya kishenzi sana, ilhali hujui kweli kwamba haupo katika ulimwengu wa wanadamu kabisa na kwamba hujidhibiti. Je, hujui kwamba maisha yako yalikandamizwa na roho hao wachafu zamani, au kwamba tabia yako ilishachafuliwa na maji machafu zamani? Je, unafikiri kwamba unaishi katika paradiso ya duniani, na kwamba uko katikati ya furaha? Je, hujui kwamba umeishi maisha pamoja na roho wachafu, na kwamba umeishi pamoja kwa amani na kila kitu ambacho wamekuandalia? Jinsi unavyoishi inawezaje kuwa na maana yoyote? Maisha yako yanawezaje kuwa na thamani yoyote? Umekuwa ukikimbia huku na kule kwa ajili ya wazazi wako, wazazi wa roho wachafu, lakini hujui kweli kuwa wale wanaokutega ni hao wazazi wa roho wachafu waliokuzaa na kukukela. Aidha, huna habari kwamba kweli ni wao ndio waliokupa uchafu wako wote; kile unachojua tu ni kwamba wanaweza kukuletea “furaha”, hawakuadibu, wala hawakuhukumu, na hususani hawakulaani. Hawajawahi kukulipukia kwa hasira, lakini wanakutendea kwa upendo na fadhila. Maneno yao huusitawisha moyo wako na kukuvutia sana kiasi kwamba unakanganyikiwa, na bila kutambua, unafyonzwa na unakuwa tayari kuwahudumia, ukigeuka kuwa njia yao ya kutoka na kuwa mtumishi wao. Huna malalamiko hata kidogo, bali uko tayari kuwafanyia kazi kama mbwa, kama farasi; unadanganywa na wao. Kwa sababu hii, huna majibu

yoyote kabisa kwa kazi Ninayoifanya. Si ajabu kwamba kila wakati wewe hutaka kuponyoka kutoka Kwangu kwa siri, na si ajabu kwamba kila wakati wewe hutaka kutumia maneno matamu kupata kibali kutoka Kwangu kwa njia danganyifu. Kama inavyotokea, tayari ulikuwa na mpango mwingine, na mpangilio mwingine. Unaweza kuona matendo Yangu kidogo kama mwenye Uweza, lakini huna ufahamu hata kidogo kuhusu hukumu na kuadibu Kwangu. Hujui kuadibu Kwangu kulianza lini; unajua tu jinsi ya kunidanganya—lakini hujui kwamba Sitastahimili ukiukaji wowote kutoka kwa mwanadamu. Kwa kuwa tayari umeweka uamuzi wako kunitumikia Mimi, sitakuacha uende. Mimi ni Mungu anayechukia uovu, na Mimi ni Mungu ambaye ana wivu kwa mwanadamu. Kwa kuwa tayari umewekelea maneno yako juu ya madhabahu, Sitakuvumilia wewe kuhudumia mabwana wawili. Je, ulifikiri ungepata upendo mwingine baada ya kuweka maneno yako juu ya madhabahu Yangu, baada ya kuyaweka mbele ya macho Yangu? Ningewezaje kuwaruhusu watu kunidanganya Mimi kwa njia hiyo? Je, ulidhani kwamba ungeweza kuweka nadhiri kikawaida, kula kiapo Kwangu Mimi na ulimi wako? Je, ungewezaje kula kiapo kwa kiti Changu cha enzi, Aliye Juu Zaidi? Je, ulifikiri kwamba viapo vyako vilikuwa tayari vimekufa? Nawaambia, hata kama miili yenu ikifa, viapo vyenu haviwezi kufa. Hatimaye, Nitawahukumu kwa msingi wa viapo vyenu. Lakini mnadhani kwamba mnaweza kuweka maneno yenu mbele Yangu ili kunivumilia Mimi na kwamba mioyo yenu inaweza kuwatumikia pepo wachafu na pepo wabaya. Je, hasira Yangu ingewezaje kuwavumilia hao watu mithili ya mbwa na nguruwe wanaonidanganya? Lazima Nitekeleze amri Zangu za kiutawala, na kuwapokonya kutoka kwa mikono ya pepo wachafu wale wote wenye fukuto, “wacha Mungu” ambao wanaamini katika Mimi “kunitumikia” Mimi kwa njia ya mpango, kuwa ng’ombe Wangu, kuwa farasi Wangu na kudhibitiwa na Mimi. Nitakufanya ushike uamuzi wako wa awali na kunitumikia Mimi tena. Siwezi kuvumilia kiumbe yeyote kunidanganya Mimi. Je, ulifikiria kwamba ungeweza kufanya maombi tu kiutukutu na kudanganya kiutukutu mbele Yangu? Je, ulifikiri kwamba Mimi sikuwa nimesikia au kuona maneno na matendo yako? Je, maneno yako na matendo yako yangekosaje kuwa katika mtazamo Wangu? Ningewezaje kuwaruhusu watu kunidanganya Mimi kwa njia hiyo?

Nimekuwa miongoni mwenu, Nimeshirikiana nanyi kwa majira kadhaa ya kuchipua na kwa majira kadhaa ya kupukutika, Nimeishi kati yenu kwa muda mrefu—ni kiasi gani cha tabia yenu ya kudharaulika kimeponyoka mbele ya macho Yangu? Maneno yenu hayo ya dhati daima yarudisha mwangwi ndani ya masikio Yangu; mamilioni na mamilioni ya matarajio yenu yamewekwa juu ya madhabahu Yangu—hayawezi hata kuhesabiwa. Lakini kwa kujitolea kwako na kile mnachokitumia, hakuna hata kidogo. Hakuna hata tone dogo la uaminifu wenu kwenye madhabahu Yangu. Yako wapi matunda ya imani yenu Kwangu? Mmepokea neema isiyo na mwisho kutoka Kwangu na mmeona mafumbo yasiyo na mwisho kutoka mbinguni, na

Nimewaonyesha hata miale ya mbinguni lakini Sijawahi kuwa na moyo wa kuwachoma, na ni kiasi gani mmenipa Mimi kama malipo? Je, mko radhi kunipa Mimi kiasi gani? Kama umeshikilia chakula Nilichokupa, unageuka na kunitolea Mimi, hata ukisema kuwa ni kitu ambacho umepata kama malipo kwa jasho la kazi yako ngumu, kwamba unatoa yote uliyo nayo Kwangu. Je, unawezaje kukosa kujua kwamba “michango” yako Kwangu ni vitu vyote vilivyoibwa kutoka kwa madhabahu Yangu? Na sasa unavitoa Kwangu—si wewe unanidanganya Mimi? Unawezaje kukosa kujua kuwa vitu Ninavyovifurahia leo ni matoleo yote juu ya madhabahu Yangu, na sicho kile ulichokichuma kama malipo ya kazi yako ngumu halafu ukanitolea Mimi? Kwa kweli mnathubutu kunidanganya Mimi kwa njia hii, kwa hiyo ni kwa jinsi gani Ninaweza kuwasamehe? Ninawezaje kuvumilia hili zaidi? Nimewapa kila kitu. Nimewafungulia kila kitu, Nikakimu mahitaji yenu, na kuyafungua macho yenu, lakini bado mnanidanganya Mimi kwa njia hii, mkipuza dhamiri yenu. Bila ubinafsi Nimewapa kila kitu, ili kwamba hata kama mnateseka, mmepata kutoka Kwangu kila kitu Nilichokileta kutoka mbinguni. Lakini hamna kujitolea kamwe, na hata kama mna mchango mdogo, mnalipa deni baada ya hapo. Je, si mchango wako utakuwa bure? Kile ambacho umenipa si chochote isipokuwa chembe moja ya mchanga, lakini kile ulichouliza kutoka Kwangu ni tani moja ya dhahabu. Je, si wewe unakuwa muhali? Ninafanya kazi miongoni mwenu. Hakuna kabisa dalili ya asilimia kumi ambayo Ninapaswa kupata, sembuse dhabihu za ziada. Zaidi ya hayo, asilimia kumi inayochangwa na wale ambao ni wacha Mungu inachukuliwa na wale waovu. Je, si nyinyi wote mmetawanyika kutoka Kwangu? Je, si nyinyi nyote mna uhasama na Mimi? Je, si nyinyi nyote mnaharibu madhabahu Yangu? Je, mtu wa aina hii anawezaje kuonekana kama hazina machoni Pangu? Je, si yeye ni nguruwe, mbwa ambao Ninawachukia? Ningewezaje kurejelea uovu wenu kama hazina? Kazi Yangu kwa kweli ni ya nani? Inawezekana kuwa tu ni ya kuwapiga nyinyi nyote ili kufichua mamlaka Yangu? Je, si maisha yenu yameshikiliwa na neno moja kutoka Kwangu? Ni kwa nini Ninatumia maneno tu kuwaagiza na Sijayageuza maneno kuwa ukweli ili kuwapiga haraka iwezekanavyo? Je, maneno Yangu na kazi Yangu ni ya kuwapiga wanadamu tu? Je, Mimi ni Mungu ambaye huwaua wasio na hatia bila ubaguzi? Hivi sasa, ni wangapi wenu ambao wako hapo mbele Yangu ambao wanatafuta njia sahihi ya maisha ya mwanadamu na nafsi zao nzima? Ni miili yenu tu iliyo mbele Yangu, lakini mioyo yenu iko huru, na iko mbali, mbali na Mimi. Kwa sababu hamjui kwa kweli kazi Yangu ni nini, kuna baadhi yenu ambao mnataka kuondoka Kwangu, mnaojitenga na Mimi, na mnataka kuishi katika mahali hapo pa raha ambapo hakuna kuadibu, hakuna hukumu. Je, hili ndilo watu wanatamani katika mioyo yao? Mimi hakika sikulazimishi. Njia yoyote utakayoichukua ni uchaguzi wako mwenyewe, na njia ya leo huenda sambamba na hukumu na laana, lakini nyote mnapaswa kujua kwamba kile Niliyowapa, iwe ni hukumu au kuadibu, zote ni zawadi bora kabisa Ninazoweza kuwapa, na vyote ni vitu ambavyo mnahitaji kwa dharura.

Kazi katika Enzi ya Sheria

Kazi ambayo Yehova alifanya kwa Waisraeli ilianzisha mahali pa Mungu pa asili miongoni mwa binadamu, ambapo pia palikuwa pahali patakatifu ambapo Alikuwapo. Aliwekea kazi Yake mipaka kwa watu wa Israeli. Mwanzoni, Hakufanya kazi nje ya nchi ya Israeli, lakini, Alichagua kikundi cha watu Aliowaona kuwa wa kufaa ili kuzuia eneo la kazi Yake. Israeli ni mahali ambapo Mungu aliwaumba Adamu na Hawa, na kutoka katika mavumbi ya mahali hapo Yehova alimuumba mwanadamu; mahali hapa pakawa kituo cha kazi Yake duniani. Waisraeli, ambao walikuwa wa ukoo wa Nuhu na pia wa ukoo wa Adamu, walikuwa msingi wa kibinadamu wa kazi ya Yehova duniani.

Wakati huu, umuhimu, kusudi na awamu za kazi ya Yehova huko Israeli zilikuwa kuanzisha kazi Yake katika dunia nzima, ambayo, ikichukua Israeli kama kituo chake, ilienea polepole hadi kwa mataifa yasiyo ya Kiyahudi. Hii ni kanuni ambayo kwayo Anafanya kazi katika ulimwengu mzima—kuunda mfano na kisha kuupanua hadi watu wote ulimwenguni watakuwa wamepokea injili Yake. Waisraeli wa kwanza walikuwa wa ukoo wa Nuhu. Watu hawa walikuwa wamejawa tu na pumzi ya Yehova, na walielewa kiasi cha kutosha ili kushughulikia mambo muhimu ya msingi ya maisha, lakini hawakujua Yehova alikuwa Mungu wa aina gani, au mapenzi Yake kwa mwanadamu, sembuse jinsi wanavyopaswa kumcha Bwana wa viumbe vyote. Kuhusu iwapo kulikuwa na sheria na kanuni za kutiwa,^[a] au iwapo kulikuwa na wajibu ambayo viumbe walioumbwa wanapaswa kumfanyia Muumba, wa ukoo wa Adamu hawakujua hata kidogo kuhusu mambo haya. Yote waliyojua ilikuwa kwamba mume anapaswa kutokwa jasho na kufanya kazi ili kukimu familia yake, na kwamba mke anapaswa kumtii mume wake na kuendeleza jamii ya binadamu ambao Yehova alikuwa ameumba. Kwa maneno mengine, watu wa aina hii, ambao walikuwa na pumzi ya Yehova na uzima Wake pekee, hawakujua kabisa kuhusu jinsi ya kufuata sheria za Mungu au jinsi ya kumridhisha Bwana wa viumbe vyote. Walielewa kidogo sana. Kwa hivyo ingawa hakukuwa na kitu kisicho kipotovu au cha udanganyifu mioyoni mwao na wivu na ugomvi viliibuka miongoni mwao mara chache, hata hivyo hawakuwa na maarifa au ufahamu wa Yehova, Bwana wa viumbe vyote. Mababu hawa wa mwanadamu walijua tu kula vitu vya Yehova, na kufurahia vitu vya Yehova, lakini hawakujua kumcha Yehova: hawakujua kwamba Yehova ndiye Yule wanayepaswa kumwabudu kwa kupiga magoti. Kwa hiyo wangeweza kuitwa viumbe Wake vipi? Kama hali ingekuwa hivi, je maneno, “Yehova ndiye Bwana wa viumbe vyote” na “Alimuumba mwanadamu ili mwanadamu aweze kumdhihirisha Yeye, kumtukuza Yeye, na kumwakilisha Yeye”—hayangekuwa yamesemwa bure? Watu ambao hawamchi Yehova wangeweza kuwa ushuhuda kwa utukufu Wake? Wangeweza kuwa dhihirisho la utukufu Wake? Je, maneno ya Yehova “Nilimuumba mwanadamu kwa mfano Wangu” si yangekuwa silaha mikononi mwa Shetani basi—yule

mwovu? Maneno haya basi hayangekuwa alama ya fedheha kwa Yehova kumuumba mwanadamu? Ili kukamilisha hatua hiyo ya kazi, baada ya kuwaumba wanadamu, Yehova hakuwaagiza au kuwaongoza kutoka wakati wa Adamu hadi ule wa Nuhu. Badala yake, baada ya dunia kuharibiwa na gharika tu ndiyo wakati ambapo Alianza rasmi kuwaongoza Waisraeli, ambao walikuwa wa ukoo wa Nuhu na pia wa Adamu. Kazi na matamshi Yake huko Israeli yaliwapa watu wote wa Israeli mwongozo walipokuwa wakiishi maisha yao katika nchi yote ya Israeli, na kwa njia hii yakaonyesha binadamu kwamba Yehova hakuweza tu kupuliza pumzi ndani ya mwanadamu, ili aweze kuwa na uhai kutoka Kwake na kuinuka kutoka mavumbini kuwa mwanadamu aliyeumbwa, lakini kwamba pia Angeweza kuwachoma wanadamu, na kuwalaani wanadamu, na kutumia fimbo Yake kuwatawala wanadamu. Kwa hivyo, pia waliona kwamba Yehova angeweza kuyaongoza maisha ya mwanadamu duniani, na kuzungumza na kufanya kazi miongoni mwa binadamu kulingana na saa za mchana na za usiku. Alifanya kazi hiyo ili tu viumbe Wake waweze kujua kwamba mwanadamu alitoka kwa mavumbi yaliyochaguliwa na Yeye, na aidha kwamba mwanadamu alikuwa ameumbwa na Yeye. Siyo haya tu, lakini kazi Aliyoanza huko Israeli ilikusudiwa ili kwamba watu na mataifa (ambao kwa kweli hawakuwa wametengwa na Israeli, lakini badala yake walikuwa wameenea kutoka kwa Waisraeli, ilhali bado walikuwa wa ukoo wa Adamu na Hawa) waweze kupokea injili ya Yehova kutoka Israeli, ili viumbe wote walioumbwa ulimwenguni waweze kuwa na uwezo wa kumcha Yehova na kumchukulia kuwa mkuu. Yehova asingeanza kazi Yake huko Israeli, lakini badala yake, baada ya kuwaumba wanadamu, awaache waishi maisha machangamfu duniani, basi katika hali hiyo, kwa sababu ya asili ya maumbile ya mwanadamu (asili inamaanisha kwamba mwanadamu hawezi kamwe kujua vitu ambavyo hawezi kuviona, yaani kwamba hangejua kwamba ilikuwa ni Yehova ambaye aliwaumba wanadamu, sembuse sababu yake kufanya hivyo), hangejua kamwe kwamba ilikuwa Yehova aliyewaumba wanadamu au kwamba Yeye ni Bwana wa viumbe vyote. Kama Yehova angemuumba mwanadamu na kumweka duniani, na kutoshughulika na yeye na kuondoka tu, badala ya kubaki miongoni mwa wanadamu ili kuwaongoza kwa kipindi cha muda, basi katika hali hiyo wanadamu wote wangukuwa wamerudi kuwa bure: hata mbingu na dunia na vitu vyote vingi Alivyoviumba, na wanadamu wote, vingerudi kuwa bure na aidha vingekanyagwa na Shetani. Kwa njia hii matakwa ya Yehova kwamba “Duniani, yaani, miongoni mwa viumbe Vyake, Anapaswa kuwa na mahali pa kusimama, mahali patakatifu” yangevunjwa. Na hivyo, baada ya kuwaumba wanadamu, kwamba Aliweza kubaki miongoni mwao kuwaongoza katika maisha yao, na kuzungumza nao kutoka miongoni mwao, yote haya yalikuwa ili kufanikisha hamu Yake, na kutimiza mpango Wake. Kazi Aliyoifanya huko Israeli ilikusudiwa tu kutekeleza mpango Aliokuwa ameuweka kabla ya kuumba Kwake vitu vyote, na kwa hivyo Yeye kufanya kazi kwanza miongoni mwa Waisraeli na Yeye kuumba vitu vyote hakukutofautiana, lakini yote yalikuwa kwa ajili ya usimamizi

Wake, kazi Yake, na utukufu Wake, na pia ili kuimarisha maana ya Yeye kuumba wanadamu. Aliyaongoza maisha ya wanadamu duniani kwa miaka elfu mbili baada ya Nuhu, wakati ambapo Aliwafunza wanadamu kuelewa jinsi ya kumcha Yehova Bwana wa viumbe vyote, jinsi ya kuendesha maisha yao na jinsi ya kuendelea kuishi, na zaidi ya yote, jinsi ya kutenda kama shahidi wa Yehova, kumtii, na kumcha, hata kumsifu kwa muziki kama Daudi na wakuhani wake walivyofanya.

Kabla ya miaka elfu mbili ambapo Yehova alifanya kazi Yake, mwanadamu hakujuu chochote, na karibu wanadamu wote walikuwa wamejipata katika upotovu, hadi, kabla ya uharibifu wa dunia na gharika, walikuwa wamefika kina cha uzinzi na upotovu ambapo mioyo yao haikuwa na Yehova, sembuse njia Yake. Hawakuelewa kamwe kazi ambayo Yehova angefanya; hawakuwa na mantiki, sembuse maarifa, na, kama mashine inayopumua, walikuwa hawamjui mwanadamu, Mungu, dunia, uhai na kadhalika kikamilifu. Duniani walishiriki katika ushawishi mwingi, kama yule nyoka, na walisema mambo mengi ambayo yalimkosea Yehova, lakini kwa sababu hawakujua Yehova hakuwaadibu au kuwafundisha nidhamu. Ni baada ya gharika tu, wakati Nuhu alikuwa na umri wa miaka 601, ndipo Yehova alijitokeza rasmi kwa Nuhu na kumwongoza yeye na familia yake, Akiongoza ndege na wanyama ambao walisalia baada ya gharika pamoja na Nuhu na ukoo wake, hadi mwisho wa Enzi ya Sheria, yote ikiwa ni miaka 2,500. Alikuwa akifanya kazi huko Israeli, yaani, alikuwa akifanya kazi kirasmi, kwa jumla ya miaka 2,000, na Alikuwa akifanya kazi huko Israeli sawia na nje ya Israeli kwa miaka 500, yote ikijumuisha miaka 2,500. Katika kipindi hiki, Aliwaagiza Waisraeli kwamba ili kumhudumia Yehova, iliwapasa kujenga hekalu, kuvaa majoho ya makuhani, na kutembea miguu mitupu kuingia hekaluni kunapopambazuka, viatu vyao visije vikachafua hilo hekalu na moto kushushwa chini kwao kutoka juu ya hekalu na kuwachoma hadi kufa. Walitekeleza wajibu wao na kutii mipango ya Yehova. Walimwomba Yehova hekaluni, na baada ya kupokea ufunuo wa Yehova, yaani, baada ya Yehova kuzungumza, waliuongoza umati na kuufunza kwamba wanapaswa kumcha Yehova—Mungu wao. Na Yehova aliwaambia kwamba ingewapasa kujenga hekalu na madhabahu, na katika wakati uliowekwa na Yehova, yaani, katika siku ya Pasaka, wangepaswa kuwatayarisha ndama na wanakondoo waliozaliwa karibuni kuwaweka juu ya madhabahu kama dhabihu kumhudumia Mungu, ili kuwazuia na kuweka uchaji kwa Yehova mioyoni mwao. Iwapo walitii sheria hii ikawa kipimo cha uaminifu wao kwa Yehova. Yehova pia aliwaagizia siku ya Sabato, siku ya saba ya uumbaji Wake. Akafanya siku baada ya Sabato kuwa siku ya kwanza, siku ya wao kumwabudu Yehova, kumtolea dhabihu, na kumtengenezea Muziki. Katika siku hii, Yehova aliwaita pamoja wakuhani wote ili kugawa dhabihu zilizokuwa juu ya madhabahu kwa ajili ya watu kula, ili wangeweza kufurahia dhabihu zilizokuwa juu ya madhabahu ya Yehova. Naye Yehova alisema kwamba walikuwa wamebarikiwa, kwamba

walishiriki sehemu na Yeye, na kwamba walikuwa wateule Wake (ambalo lilikuwa agano la Yehova na Waisraeli). Hii ndiyo maana, hadi siku ya leo, watu wa Israeli bado wanasema kwamba Yehova ni Mungu wao pekee, na si Mungu wa watu wengine.

Katika Enzi ya Sheria, Yehova aliweka amri nyingi za Musa kupitisha kwa Waisraeli waliomfuata kutoka Misri. Amri hizi walipewa Waisraeli na Yehova, na hazikuwa na uhusiano kwa Wamisri: zilinuiwa kuwazuia Waisraeli. Yeye alizitumia amri kuwatolea madai. Iwapo waliishika Sabato, iwapo waliwaheshimu wazazi wao, iwapo waliziabudu sanamu, na kadhalika: hizi zilikuwa kanuni ambazo kwazo walihukumiwa kuwa wenye dhambi au wenye haki. Miongoni mwao, kuna baadhi walioangamizwa kwa moto wa Yehova, baadhi waliopigwa mawe hadi kufa, na baadhi waliopokea baraka za Yehova, na haya yaliamuliwa kulingana na iwapo walizitii amri hizi au la. Wale ambao hawakuishika Sabato wangepigwa mawe hadi kufa. Wale makuhani ambao hawakuishika Sabato wangeangamizwa na moto wa Yehova. Wale ambao hawakuwaheshimu wazazi wao pia wangepigwa mawe hadi kufa. Yote haya yalikubaliwa na Yehova. Yehova alianzisha amri na sheria Zake ili, Alipokuwa akiwaongoza katika maisha yao, watu wangesikiliza na kuti neno Lake na kutoasi dhidi Yake. Alitumia sheria hizi kuidhibiti jamii ya binadamu iliyokuwa imezaliwa karibuni, ili kuweka vizuri zaidi msingi wa kazi Yake ya baadaye. Na kwa hivyo, kwa msingi wa kazi ambayo Yehova alifanya, enzi ya kwanza iliitwa Enzi ya sheria. Ingawa Yehova alisema matamshi mengi na kufanya kazi nyingi, Aliwaongoza watu kwa njia njema tu, akiwafunza watu hawa wasiojua jinsi ya kuwa binadamu, jinsi ya kuishi, jinsi ya kuelewa njia ya Yehova. Kwa kiwango kikubwa sana, kazi Aliyoifanya ilikuwa ili kuwasababisha watu kutii njia Yake na kufuata sheria Zake. Kazi hii ilifanywa kwa watu waliokuwa wamepotoshwa kwa kiasi kidogo; haikuenea kiasi cha kubadili tabia yao au maendeleo katika maisha. Alijishughulisha tu na kutumia sheria kuwazuia na kuwadhibiti watu. Kwa Waisraeli wa wakati huo, Yehova alikuwa Mungu katika hekalu tu, Mungu huko mbinguni. Alikuwa nguzo ya wingu, nguzo ya moto. Yote ambayo Yehova aliwataka wafanye ilikuwa ni kutii kile ambacho watu wa leo wanakijua kama sheria na amri Zake—mtu anaweza pia kusema kanuni—kwa sababu kile ambacho Yehova alifanya hakikunuiwa kuwabadilisha, ila kuwapa vitu zaidi ambavyo mwanadamu anapaswa kuwa navyo, kuwaagiza kutoka kinywani Mwake mwenyewe, kwa sababu baada ya kuumbwa, mwanadamu hakuwa na chochote alichopaswa kumiliki. Na kwa hivyo, Yehova aliwapa watu vitu ambavyo walipaswa kumiliki kwa ajili ya maisha yao duniani, Akiwafanya watu Aliokuwa ameongoza kuwashinda mababu zao, Adamu na Hawa, kwa sababu kile Yehova alichowapa kilishinda kile Alichokuwa amewapa Adamu na Hawa mwanzoni. Bila kujali, kazi ambayo Yehova alifanya huko Israeli ilikuwa tu kuwaongoza binadamu na kuwafanya binadamu wamtambue Muumba wao. Hakuwashinda wala kuwabadilisha, ila Aliwaongoza tu. Hii ndiyo kazi yote ya Yehova katika Enzi ya Sheria. Ndio

usuli, masimulizi ya kweli, kiini cha kazi Yake katika nchi nzima ya Israeli, na mwanzo wa kazi Yake ya miaka elfu sita—kuendeleza udhibiti wa wanadamu kwa mkono wa Yehova. Kutokana na hili kulizaliwa kazi zaidi katika mpango Wake wa usimamizi wa miaka elfu sita.

Tanbihi:

a. Maandishi ya asili hayana maneno “kutiwa”.

Maelezo ya Kweli ya Kazi Katika Enzi ya Ukombozi

Mpango Wangu mzima wa usimamizi, mpango ambao una urefu wa miaka elfu sita, unashirikisha hatua tatu, au enzi tatu: Enzi ya Sheria mwanzoni; Enzi ya Neema (ambayo pia ni Enzi ya Ukombozi); na katika siku za mwisho, Enzi ya Ufalme. Kazi Yangu katika enzi hizi tatu hutofautiana katika maudhui kulingana na asili ya kila enzi, lakini katika kila hatua huambatana na mahitaji ya mwanadamu—au, kwa usahihi zaidi, inafanywa kulingana na ujanja ambao Shetani hutumia katika vita Vyangu dhidi yake. Madhumuni ya Kazi Yangu ni kumshinda Shetani, ili kudhihirisha hekima Yangu na kudura, kufichua ujanja wote wa Shetani na hivyo kuokoa wanadamu wote, wanaoishi chini ya miliki yake. Ni ili kuonyesha hekima Yangu na kudura na wakati uo huo kufichua ubovu wa Shetani usiovumilika. Aidha, ni ili kufundisha viumbe Wangu kubagua kati ya mema na mabaya, kutambua kwamba Mimi ndiye Mtawala wa vitu vyote, kuona wazi kwamba Shetani ni adui wa binadamu, wa chini kuliko wote, yule mwovu, na kujua, kwa uhakika kabisa tofauti kati ya mema na mabaya, ukweli na uwongo, utakatifu na uchafu, kilicho kikuu na kilicho cha aibu. Kwa njia hii, binadamu wasiofahamu wataweza kunishuhudia kwamba si Mimi Ninayewapotosha wanadamu, na kwamba ni Mimi tu—Bwana wa viumbe—Ninayeweza kumwokoa binadamu, Ninayeweza kumpa mwanadamu vitu kwa ajili ya raha yake; na atapata kujua kwamba Mimi Ndimi Mtawala wa vitu vyote na Shetani ni mmoja tu wa viumbe niliowaumba na ambaye baadaye alinigeuka. Mpango Wangu wa usimamizi wa miaka elfu sita umegawanywa katika hatua tatu ili kufikia matokeo yafuatayo: kuruhusu viumbe Wangu wawe mashahidi Wangu, kuelewa mapenzi Yangu, na wajue kwamba Mimi Ndimi ukweli. Hivyo, wakati wa awamu ya kwanza ya kazi ya katika Mpango Wangu wa usimamizi wa miaka elfu sita, Nilifanya kazi ya sheria, ambayo ilikuwa ndiyo kazi ambayo kwayo Yehova aliwaongoza watu Wake. Hatua ya pili ilianzisha kazi ya Enzi ya Neema katika vijiji vya Yudea. Yesu Anawakilisha kazi yote ya Enzi ya Neema; Alipata mwili na kusulubiwa, na pia Akazindua Enzi ya Neema. Alisulubiwa ili kukamilisha kazi ya ukombozi, ili kumaliza Enzi ya Sheria na kuanzisha Enzi ya Neema, na hivyo Yeye Aliitwa “Kamanda Mkuu”, “Sadaka ya Dhambi,” “Mkombozi.” Kwa hiyo kazi ya Yesu ilitofautiana katika maudhui na kazi ya Yehova, ingawa zilikuwa sawa katika kanuni. Yehova Alianzisha Enzi ya Sheria, Akaunda msingi wa nyumbani, yaani, mahali pa asili, pa kazi Yake hapa duniani, na Akatoa amri na

sheria. Hizi ndizo sehemu mbili za kazi Aliyotekeleza, na zinawakilisha Enzi ya Sheria. Kazi ya Yesu katika Enzi ya Neema haikuwa kutoa sheria bali kuzitimiza, na hivyo kukaribisha Enzi ya Neema na kuhitimisha Enzi ya Sheria ambayo ilidumu kwa miaka elfu mbili. Alikuwa mwanzilishi, aliyekuja ili kuianzisha Enzi ya Neema, ilhali ukombozi ulibakia msingi wa kazi Yake. Na hivyo mafanikio Yake yalikuwa pia mara mbili: kufungua enzi mpya, na kukamilisha kazi ya ukombozi kupitia kusulubiwa Kwake, nakisha Akaondoka. Na hapo ndipo Enzi ya Sheria ilifikia mwisho wake na Enzi ya Neema ikaanza.

Kazi ambayo Yesu alifanyika ililingana na mahitaji ya mwanadamu katika enzi hiyo. Kazi Yake ilikuwa ni kuwakomboa wanadamu, kuwasamehe dhambi zao, na kwa hivyo tabia Yake yote ilikuwa ya unyenyekevu, uvumilivu, upendo, ucha Mungu, ustahamilivu, huruma na wema. Aliwabariki wanadamu kwa wingi na kuwaletea neema nyingi, na mambo yote ambayo wangeweza kufurahia, Aliwapa kwa ajili ya furaha yao: amani na furaha, uvumilivu Wake na upendo, huruma Yake na wema. Katika siku hizo, chote alichokutana nacho mwanadamu kilikuwa wingi wa vitu vya kufurahia tu: Moyo wake ulikuwa na amani na uhakikisho, roho yake ilifarijika, na alikuwa anaruzukiwa na Mwokozi Yesu. Sababu iliyomfanya mwanadamu aweze kufaidi mambo haya ni matokeo ya enzi alimoishi. Katika Enzi ya Neema mwanadamu alikuwa amepotoshwa tayari na Shetani, na hivyo kazi ya ukombozi wa wanadamu wote ulihitaji neema nyingi, ustahimili na uvumilivu usio na mwisho, na hata zaidi, sadaka ya kutosha kulipia dhambi za wanadamu, ili kufikia athari yake. Kile wanadamu walichoona katika Enzi ya Neema kilikuwa tu sadaka Yangu ya kulipia dhambi za binadamu, yaani, Yesu. Yote waliyojua ni kwamba Mungu angeweza kuwa mwenye huruma na uvumilivu, na yote waliyoona ni huruma ya Yesu na wema Wake. Hii yote ilikuwa ni kwa sababu wao walizaliwa katika Enzi ya Neema. Na hivyo, kabla ya kuweza kukombolewa, walilazimika kufurahia neema za aina nyingi ambazo Yesu aliwapa; hili pekee ndilo lilikuwa la manufaa kwao. Kwa njia hii, wangeweza kusamehewa dhambi zao kupitia kufurahia kwao neema, na pia wangeweza kuwa na nafasi ya kukombolewa kupitia kufurahia ustahimili wa Yesu na uvumilivu. Ni kwa njia ya ustahimili wa Yesu na uvumilivu pekee ndio walipata haki ya wa kupokea msamaha na kufurahia neema nyingi kutoka kwa Yesu—kama vile Yesu alivyosema: Sijakuja kuwakomboa wenye haki, ila wenye dhambi, kukubali dhambi zao zisamehewe. Kama Yesu angepata mwili wa tabia ya hukumu, laana, na kutovumilia makosa ya mwanadamu, basi mwanadamu kamwe hangeweza kupata nafasi ya kukombolewa, na daima yeye angebaki mwenye dhambi. Hali ingekuwa hivi, mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita ungekoma katika Enzi ya Sheria na Enzi ya Sheria ingeendelea kwa miaka elfu sita. Dhambi za mwanadamu zingengezeko zaidi na kuwa mbaya zaidi tu, na uumbaji wa binadamu ungekuwa wa bure. Wanadamu wangeweza tu kumtumikia Yehova chini ya sheria, bali dhambi zao zingezidi za wanadamu wa kwanza kuumbwa. Jinsi Yesu

alivyowapenda wanadamu zaidi, Akisamehe dhambi zao na kuwapa huruma na wema wa kutosha, ndivyo wanadamu walizidi kuwa na uwezo wa kuokolewa, wa kuitwa wanakondoo waliopotea ambao Yesu Aliwanunua tena kwa gharama kubwa. Shetani hakuweza kuingilia katika kazi hii, kwa sababu Yesu Aliwatunza wafuasi Wake kama mama mwenye upendo anavyotunza mtoto mchanga aliye kifuani pake. Yeye hakuwa na hasira nao au kuwadharau, bali Alikuwa Amejaa faraja; Yeye kamwe hakuwa na ghadhabu miongoni mwao, lakini alistahimili dhambi zao na Akapuza upumbavu wao na kutofahamu, hata kusema, “Uwasamehe wengine mara sabini mara saba.” Kwa hiyo moyo Wake ulirekebisha mioyo ya wengine. Ilikuwa ni kwa njia hii ndiyo watu walipokea msamaha wa dhambi kupitia uvumilivu Wake.

Ingawa Yesu katika mwili Wake hakuwa na hisia kabisa, Yeye daima Aliwafariji wanafunzi Wake, Aliwapa mahitaji yao, Akawasaidia, na Akawaruzuku. Bila kujali kiwango cha kazi Alichofanya au kiasi gani cha mateso Alivumilia, Yeye kamwe hakuwa na matarajio ya kupita kiasi kwa mwanadamu, lakini kila mara Alikuwa mwenye subira na kuvumilia dhambi zao, kiasi kwamba katika Enzi ya Neema kwa upendo watu walimwita “Mwokozi Yesu anayependeka.” Kwa watu wa wakati huo—kwa watu wote—kile Yesu Alikuwa nacho na kile Alichokuwa, kilikuwa huruma na wema. Yeye kamwe hakukumbuka dhambi za, na hakuwatendea kulingana na dhambi zao. Kwa sababu hiyo ilikuwa enzi tofauti, mara nyingi Alitoa chakula na vinywaji kwa watu ili waweze kula hadi washibe. Yeye Aliwatendea wafuasi Wake wote kwa ukarimu, akaponya wagonjwa, kufukuza mapepo na kufufua wafu. Ili kwamba watu waweze kumwamini na kuona kwamba yote Aliyofanya yalifanyika kwa bidii na kwa dhati, Yeye Alifika kiwango cha kufufua maiti iliyooza, kuwaonyesha kwamba mikononi Mwake hata wafu wanaweza kuwa hai tena. Kwa njia hii Alivumilia kwa kimya na kufanya kazi Yake ya ukombozi kati yao. Hata kabla Asulubiwe, Yesu Alikuwa tayari Amebeba dhambi za binadamu na kuwa sadaka ya dhambi kwa ajili ya wanadamu. Hata kabla Asulubiwe, Alikuwa tayari Amefungua njia ya msalaba ili kuwakomboa wanadamu. Mwishowe Aligongwa misumari msalabani, Alijitoa sadaka Yeye Mwenyewe kwa ajili ya msalaba, na Alitoa huruma Yake yote, wema Wake, na utakatifu kwa wanadamu. Kwa wanadamu daima alikuwa mvumilivu, kamwe Hakutafuta kulipiza kisasi, lakini Aliwasamehe dhambi zao, Akiwasihi watubu, na kuwafundisha kuwa na subira, uvumilivu na upendo, kufuata nyayo Zake na kujitoa wenyewe kwa ajili ya msalaba. Upendo Wake kwa ndugu ulizidi upendo Wake kwa Maria. Kanuni ya kazi Aliyofanya ilikuwa kuwaponya watu na kutoa mapepo, yote kwa ajili ya ukombozi Wake. Haijalishi Alikoenda, Yeye Aliwatendea wote waliomfuata kwa neema. Aliwafanya maskini kuwa tajiri, viwete watembee, vipofu waone na viziwi wasikie; Yeye hata Aliwaalika watu wa hadhi ya chini kabisa, maskini zaidi, wenye dhambi, kula pamoja naye, Akikosa kuwaepuka kamwe ila daima Alikuwa na subira, hata kusema: Wakati mchungaji anampoteza kondoo mmoja kati ya mia,

yeye ataondoka na kuwaacha nyuma wale tisini na tisa ili amtafute kondoo mmoja aliyepotea, na anapompata yeye atafurahia sana. Yeye Aliwapenda wafuasi Wake kama kondoo anavyopenda wanakondoo wake. Ingawa walikuwa wajinga na wasio na ufahamu, na walikuwa wenye dhambi katika macho Yake, na zaidi walikuwa washirika wa chini zaidi katika jamii, Aliona hawa wenye dhambi—waliodharauliwa na wengine—kama vipenzi Vyake. Kwa kuwa Aliwapendelea, Alitoa uhai Wake kwa ajili yao, kama mwana kondoo alitolewa madhabahuni. Alitembea kati yao kama mtumishi wao, Akiwaruhusu kumtumia na kumchinja, Alijinyenyekeza kwao bila masharti. Kwa wafuasi Wake Alikuwa Mwokozi Yesu aliyependeka, lakini kwa Mafarisayo, ambao waliwahubiria watu kutoka viweko virefu vya mnara, Hakuonyesha huruma na wema, bali chuki na maudhi. Hakufanya kazi nyingi miongoni mwa Mafarisayo, Akiwahubiria na kuwakemea mara chache tu; Yeye hakutembea miongoni mwao akifanya kazi ya ukombozi, au kufanya ishara na maajabu. Alitoa huruma Yake na wema Wake wote kwa wafuasi Wake, akivumilia kwa ajili ya hawa wenye dhambi mpaka mwisho kabisa, wakati Alipigwa misumari msalabani na akastahimili kila udhalilishaji mpaka Alivyowakomboa wanadamu wote kikamilifu. Hii ndiyo ilikuwa kazi Yake yote.

Bila ukombozi wa Yesu, wanadamu wangeishi milele katika dhambi, na kuwa watoto wa dhambi, kizazi cha mapepo. Kama ingeendelea hivyo, dunia yote ingekuwa mahali pa kulala pa Shetani, maskani yake. Lakini kazi ya ukombozi ilihitaji kuonyesha huruma na wema kwa wanadamu; kupitia kwa njia hiyo tu ndio wanadamu wangeweza kupokea msamaha na mwishowe kupata haki ya kukamilishwa na kumilikiwa kikamilifu. Bila hatua hii ya kazi, mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita haungeweza kuendelea mbele. Kama Yesu hangesulubiwa, kama Yeye Angewaponya tu watu na kufukuza mapepo, basi watu hawangesamehewa dhambi zao kikamilifu. Katika miaka mitatu na nusu ambayo Yesu Alitumia kufanya kazi Yake hapa duniani alikamilisha tu nusu ya kazi Yake ya ukombozi; kisha, kwa kupigiliwa misumari msalabani na kuwa mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kukabidhiwa kwa yule mwovu, Yeye Alikamilisha kazi ya kusulubiwa na Akaendesha majaaliwa ya wanadamu. Baada ya Yeye kukabidhiwa mikononi mwa Shetani tu, ndipo alipowakomboa wanadamu. Kwa miaka thelathini na mitatu na nusu Aliteseka duniani, Akidhihakiwa, kukashifiwa, na kuachwa, kiasi cha Yeye kukosa mahali pa kulaza kichwa chake, mahali pa kupumzika; kisha Akasulubiwa, huku nafsi Yake yote—mwili mtakatifu na usio na hatia—kupigiliwa misumari msalabani. Alivumilia kila namna ya mateso yaliyoko. Wale waliokuwa madarakani wakamdhihaki na kumcharaza mijeledi, na maaskari hata wakamtemea mate usoni; ilhali Alibaki kimya na kuvumilia mpaka mwisho, Akinyenyekea bila masharti mpaka wakati wa kifo, ambapo Yeye Alikomboa wanadamu wote. Hapo tu ndipo Aliruhusiwa kupumzika. Kazi ambayo Yesu alifanya inawakilisha tu Enzi ya Neema; haiwakilishi Enzi ya Sheria wala si mbadala wa kazi ya

siku za mwisho. Hiki ndicho kiini cha kazi ya Yesu katika Enzi ya Neema, enzi ya pili ambayo wanadamu wamepitia—Enzi ya Ukombozi.

Maneno kwa Vijana na kwa Wazee

Nimeteketeza kazi nyingi sana duniani na Nimetembea kati ya wanadamu kwa miaka mingi sana. Ilhali watu kwa nadra sana huwa na ufahamu wa sura Yangu na tabia Yangu, na watu wachache wanaweza kuelezea kikamilifu kazi Ninayofanya. Watu wanakosa mengi sana, daima wanakosa ufahamu wa kile Ninachokifanya, na mioyo yao daima iko tayari kana kwamba wanaogopa sana Nitawaleta katika hali nyingine na kisha kuwapuuza. Kwa hivyo, mtazamo wa watu Kwangu daima ni vuvuwaa pamoja na tahadhari kubwa sana. Hili ni kwa sababu watu wamekuja kwa wakati wa sasa bila kuelewa kazi Ninayofanya, na wao hasa hukanganywa na maneno ambayo Ninawaambia. Wao huyabeba maneno Yangu mikononi mwao, wasijue kama wanapaswa kujitahidi kuamini au kama wanapaswa kuyasahau kwa shaka. Hawajui kama wanapaswa kuyatia katika vitendo, au kama wanapaswa kungoja kuona. Hawajui kama wanapaswa kuachana na kila kitu na kisha kufuata kwa ujasiri, au kama wanapaswa kuendelea kuwa wa kirafiki na ulimwengu kama hapo awali. Ulimwengu wa ndani wa watu ni wenye utata sana, na wao ni wajanja sana. Kwa sababu watu hawawezi kuyaona kwa dhahiri maneno Yangu na hawawezi kuyaona kikamilifu, wengi wao wana wakati mgumu kuyatenda, na wana shida kuweka moyo wao mbele Yangu. Ninayaelewa kwa kina matatizo yenu. Udhaifu mwingi hauepukiki wakati mtu anapoishi ndani ya mwili, na vipengele vingi ya kuhusu mambo huwaletea shida. Mnalisha familia zenu, mnatumia siku zenu mkifanya kazi kwa bidii, na wakati hupita vigumu. Kuna shida nyingi za kuishi katika mwili—Sikatai hili, na bila shaka mahitaji Yangu kwenu yanalingana na shida zenu. Mahitaji katika kazi Ninayofanya yote yana msingi katika kimo chenu halisi. Labda wakati watu walipokuwa wakifanya kazi zamani mahitaji yao kwenu yalichanganywa na dalili za uziada, lakini mnapaswa kujua kwamba Sijawahi kuwa na mahitaji ya ziada kwenu katika yale Ninayosema na kutenda. Yote yanahitajika kulingana na asili ya watu, mwili, na kile wanachohitaji. Mnapaswa kujua, na Naweza kuwaambia kwa dhahiri sana, kwamba Sikupingi kufikiria fulani kwa maana kwa watu na Sipingi asili ya kimaumbile ya binadamu. Ni tu kwa sababu watu hawaelewi kwa kweli kile kilicho kiwango cha mahitaji Yangu kwao, wala hawaelewi maana ya asili ya maneno Yangu ambayo hadi sasa, watu bado wana wasiwasi na maneno Yangu, na hata chini ya nusu ya watu huyaamini maneno Yangu. Waliosalia ni wasioamini, na hata zaidi ni wale wanaopenda kunisikia “Nikisimulia hadithi.” Aidha, kuna wengi ambao hufurahia tukio hilo. Ninawapa onyo: Maneno Yangu mengi tayari yamefunguliwa kwa wale wanaoniamini Mimi, na wale ambao wanafurahia mandhari mazuri ya ufalme lakini wamefungiwa nje ya lango lake tayari wameondolewa na Mimi. Je, nyinyi si magugu tu ambavyo yamechukiwa na kukataliwa na Mimi? Je, Mngeniaga vipi na

kisha kukaribisha kurudi Kwangu kwa furaha? Nawaambieni, baada ya watu wa Ninawi kusikia maneno ya hasira ya Yehova, mara moja walitubu kwa magunia na majivu. Ilikuwa kwa sababu waliyaamini maneno Yake kwamba walijawa na woga na hofu na wakatubu kwa magunia na majivu. Na ingawa watu wa leo pia wanaamini maneno Yangu na hata zaidi kuamini kuwa Yehova amekuja tena kati yenu leo, mtazamo wenu sio chochote ila usioheshimu vitu vitakatifu, kana kwamba mnamwangalia tu Yesu aliyezaliwa Yudea maelfu kadhaa ya miaka iliyopita na sasa Ameshuka katikati yenu. Ninaelewa kabisa udanganyifu ulio ndani ya mioyo yenu; wengi wenu hunifuata kutokana na udadisi na mmekuja kunitafuta kutokana na utupu. Wakati matakwa yenu ya tatu yanavunjwawunjwa—kwa ajili ya maisha ya amani na yenye furaha—udadisi wenu pia unatapanywa. Udanganyifu ulio ndani ya mioyo ya kila mmoja wenu wote hufunuliwa kupitia maneno na matendo yenu. Kusema kweli, nyinyi mnataka tu kujua kunihusu, hamwogopi; hamjali matamshi yenu, na mnazuia tabia zenu hata mara chache zaidi. Basi imani yenu iko vipi kwa kweli? Je, ni ya kweli? Mnatumia tu maneno Yangu kuondoa wasiwasi wenu na kupunguza uchoshi wenu, ili kujaza nafasi zilizobaki tupu katika maisha yako. Ni nani miongoni mwenu ambaye ameyatia katika vitendo? Nani ana imani ya kweli? Mnaendelea kupiga kelele kwamba Mungu ni Mungu ambaye huona ndani kabisa ya mioyo ya watu, lakini ni vipi Mungu mnayepiga kelele kuhusu mioyoni mwenu analingana na Mimi? Kwa kuwa mnapiga kelele kwa njia hii, basi kwa nini mnatenda kwa njia ile? Inaweza kuwa kwamba huu ndio upendo mnaotaka kunilipizia nao? Hakuna kiasi kidogo cha upendo kwenye midomo yenu, lakini ziko wapi dhabihu zenu, na matendo yenu mema? Isingalikua maneno yenu kuyafikia masikio Yangu, Ningaliwezaje kuwachukia sana? Ikiwa kweli mliniaminia, mngewezaje kuangukia hali kama hii ya dhiki? Mnazo sura za huzuni kwenye nyuso zenu kana kwamba mko kuzimu mkishtakiwa. Hamna uhai wowote, na mnanena kuhusu sauti yenu ya ndani kwa udhaifu; mmejawa hata na malalamiko na laana. Mlipoteza imani katika yale Nifanyayo zamani na hata imani yenu ya asili imepotea, basi mnawezaje kufuata mpaka mwisho? Mnawezaje kuokolewa kwa njia hii?

Ingawa kazi Yangu ni yenye msaada mkubwa kwenu sana, maneno Yangu daima hushindwa kuwashawishi na kutofanikiwa ndani yenu. Ni vigumu kupata chombo cha kukamilishwa na Mimi na leo karibu Nimepoteza tumaini kwenu. Nimetafuta kati yenu kwa miaka kadhaa lakini ni vigumu kupata msiri. Ninahisi kama Sina imani ya kuendelea kufanya kazi ndani yenu, na Sina upendo kuendelea kuwapenda. Hili ni kwa sababu Nilikuwa Nimechukizwa kitambo na yale mafanikio yenu madogo ya kusikitisha; ni kana kwamba Sikuwahi kuzungumza kati yenu na Sikuwahi kufanya kazi ndani yenu. Mafanikio yenu yanachafua moyo sana—daima mmetiwa fedheha na karibu hamna thamani yoyote. Kwa nadra Ninapata mfano wa mwanadamu ndani yenu au kusikia harufu ya mwanadamu. Iko wapi harufu yenu mpya? Iko wapi gharama ambayo

mmelipa kwa miaka mingi, na matokeo yako wapi? Hamjawahi kuyapata? Kazi Yangu sasa ina asili mpya, mwanzo mpya. Ninaenda kutekeleza mipango mikubwa na Ninataka kutekeleza kazi kubwa, ilhali bado mnavingirika katika matope kama hapo awali, kuishi katika maji machafu ya zamani, na kwa utendaji hamjatupa mashaka yenu ya awali. Kwa hivyo, bado hamjapata chochote kutoka kwa maneno Yangu. Bado hamjatupa pahali penu pa awali pa matope na maji machafu, na mnayajua maneno Yangu tu, lakini kwa kweli hamjaingia katika eneo la uhuru wa maneno Yangu, hivyo maneno Yangu hayajawahi kufunguliwa kwenu, na yako kama kitabu cha unabii ambacho kimefungwa kwa maelfu ya miaka. Ninaonekana kwenu katika maisha yenu lakini daima hamjui, na hamnitambui hata. Takriban nusu ya maneno Ninayoyasema ni hukumu ya nyinyi, na hayo hufanikisha tu nusu ya athari ambayo yanapaswa kufanikisha, ambayo ni kutia hofu kuu ndano yenu. Nusu iliyobaki ni maneno ya kuwafundisha kuhusu maisha na jinsi ya kutenda, lakini ni kana kwamba hayapo kwenu, na kana kwamba nyinyi mnasikiliza maneno ya watoto wanaocheza, ambayo daima nyinyi huyatolea tabasamu iliyofichwa, na kisha hakuna kitu kinachofanywa. Hamjawahi kujishughulisha na mambo haya; daima mmefuata matendo Yangu kutokana na udadisi wenu ili kwamba sasa mmeanguka gizani na hamwezi kuuona mwanga—mnalia kwa huruma gizani. Kile Ninachotaka ni utiifu wenu, utiifu wenu usio na masharti na hata zaidi, Nahitaji kwamba muwe na hakika kabisa juu ya kila kitu Ninachosema. Hampaswi kukubali mtazamo wa kutokujali na hasa hampaswi kuuvumilia kwa kuchagua, ni wazi kwamba nyinyi daima hamjali maneno Yangu na kazi Yangu. Kazi Yangu inafanywa katikati yenu na Nimewapa maneno Yangu mengi, lakini mkinilaghai kwa njia hii, Ninaweza tu kutoa bure kile ambacho hamjapata na hamjatia katika vitendo kwa familia za Mataifa. Ni nini kati ya uumbaji hakipo mikononi Mwangu? Wengi wa wale kati yenu ni wa “wa miaka mingi sana” na hamna nguvu ya kukubali aina hii ya kazi Yangu. Nyinyi ni kama ndege wa Hanhao^[a], mnaishi kwa shida, na hamjawahi kuyachukulia maneno Yangu kwa uzito. Vijana ni bure sana na wanajifurahisha sana na hata zaidi wanaipuuza kazi Yangu. Hawahisi kufurahia vyakula vitamu vya karamu Yangu; Wao ni kama ndege mdogo ambaye ameruka nje ya tundu lake kwenda mbali kabisa. Je, wazee na vijana wa aina hii wanawezaje kuwa na manufaa Kwangu? Wale wa umri uliosonga wako tayari kuyatumia maneno Yangu kama kiinua mgongo mpaka wakati wako katika makaburi yao, ili baada ya wao kufa nafsi zao zinaweza kwenda juu mbinguni, na hilo linatosha. Ndiyo sababu kwa sasa, wanathamini “tamanio kubwa” na “wanajiamini sana.” Ingawa wamejawa uvumilivu kwa kazi Yangu, na wao ni waadilifu na wasiokubali kushindwa kama roho ya mtu mzee ambaye hataburutwa au kushindwa na mtu yeyote au kitu chochote kama tu ngome isiyoingilika, imani ya watu hawa siyo iliyojaa roho ya ushirikina ya maiti? Iko wapi njia yao? Kwao, njia yao siyo ndefu sana, ya mbali sana? Wangejuaje mapenzi Yangu? Hata kama imani yao ni ya kustahili kusifiwa, ni wangapi kati ya wazee hawa hawafuati kwa njia ya kuchanganyikiwa bali wanafukuzia maisha? Ni wangapi

wanaofahamu kwa kweli umuhimu wa kweli wa kazi Yangu? Nia ya nani siyo kwamba waweze kunifuata katika ulimwengu huu leo, na katika siku za karibu za usoni hawatashuka kuzimu bali kuletwa kwatika eneo jingine na Mimi? Je, mnafikiri hatima yenu ni jambo rahisi sana? Ingawa nyinyi vijana wote ni kama simba wachanga, kwa nadra mnakuwa na njia ya kweli mioyoni mwenu. Ujana wenu hauwezi kuwapa nafasi ya kupata kazi Yangu zaidi; kinyume na hilo, daima nyinyi husababisha chuki Yangu kwenu. Ingawa nyinyi ni wachanga, ama mnakosa uhai au hamna tamaa ya makuu, daima nyinyi hamjihusishi na siku zenu zijazo; ni kana kwamba hamjali, na pia mnawaza sana. Ingeweza kusemwa kuwa uchangamfu, maadili, na msimamo yanayochukuliwa ambayo yanapaswa kupatikana kwa vijana hayawezi kabisa kupatikana kwenu; nyinyi, vijana wa aina hii, mnakosa msimamo na hamna uwezo wa kutofautisha kati ya sahihi na isiyo sahihi, mema na maovu, mazuri na mabaya. Haiwezekani kupata dalili zozote zenu ambazo ni mpya. Nyinyi karibu mmejitwa na wakati kabisa, na nyinyi, vijana wa aina hii, pia mmejifunza kukubali tu, kuwa bila mantiki. Hamwezi kamwe kutofautisha kwa dhahiri mazuri kutoka kwa mabaya, hamwezi kutofautisha kati ya ukweli na uongo katika masuala, kamwe hamjitahidi kupata ubora, wala hamwezi kusema nini ni sahihi na nini si sahihi, nini ni ukweli, na nini ni unafiki. Ndani yenu kunabakia mipulizo ya ghafla ya dini hata zaidi na hata mikubwa zaidi kuliko kwa watu wazee. Nyinyi hata ni wenye kiburi na msio na busara, nyinyi ni wa ushindani, na kupenda kwenu uchokozi ni mzito sana—kijana wa aina hii anawezaje kumiliki ukweli? Mtu asiyeweza kuchukua msimamo anawezaje kushuhudia? Mtu asiye na uwezo wa kutofautisha kati ya yaliyo sahihi na yasiyo sahihi anawezaje kuitwa kijana? Mtu asiye na uhai, nguvu, utulivu, ubichi, utulivu na udhabiti wa kijana anawezaje kuitwa mfuasi Wangu? Mtu asiye na ukweli wowote wala hisia ya haki, lakini hupenda kucheza na kupigana anawezaje kufaa kuwa shahidi Wangu? Macho ambayo yamejaa uongo na chuki bila sababu kwa watu siyo wanayopaswa kuwa nayo vijana, na wale wanaotekeleza vitendo vya uharibifu, vinavyochukiza mno hawapaswi kuwa vijana. Hawapaswi kuwa bila maadili, matarajio, au tabia ya maendeleo ya shauku; hawapaswi kuvunjika moyo juu ya matarajio yao wala hawapaswi kupoteza matumaini maishani au kupoteza imani katika siku zijazo; wanapaswa kuwa na uvumilivu kuendelea na njia ya ukweli ambayo sasa wamechagua kufanikisha matamania yao ya kutumia maisha yao yote kwa ajili Yangu; hawapaswi kuwa bila ukweli, wala kuficha unafiki na udhalimu, bali wanapaswa kusimama imara katika msimamo unaofaa. Hawapaswi tu kuzurura, bali wanapaswa kuwa na roho ya kuthubutu kujitolea mhanga na kujitahidi kwa ajili ya haki na ukweli. Vijana wanapaswa kuwa na ujasiri wa kutoshindwa na ukandamizaji wa nguvu za giza na kubadili umuhimu wa uwepo wao. Vijana hawapaswi kukubali shida bila kulalamika, bali wanapaswa wawe wazi na wa kusema bila kuficha, na roho ya msamaha kwa ndugu wao. Bila shaka haya ni mahitaji Yangu ya kila mtu pamoja na ushauri Wangu kwa kila mtu. Hata zaidi, ni maneno Yangu ya kutuliza kwa vijana wote. Mnapaswa kutenda kulingana na maneno Yangu.

Hasa vijana hawapaswi kuwa bila azimio la utambuzi katika masuala, na la kutafuta haki na ukweli. Yale mnayopaswa kufuata ni mambo yote mazuri na mema, na mnapaswa kupata uhalisi wa mambo yote mazuri, na pia kuwajibika juu yaa maisha yenu—hampaswi kuyachukulia kwa wepesi. Watu huja duniani na ni nadra kupatana na Mimi, na pia ni nadra kuwa na fursa ya kutafuta na kupata ukweli. Kwa nini msithamini wakati huu mzuri kama njia sahihi ya kutafuta katika maisha haya? Na ni kwa nini daima nyinyi hupuuza sana ukweli na haki? Kwa nini daima nyinyi hujikanyaga na kujiangamiza kwa ajili ya ule udhalimu na uchafu ambao huchezea watu? Na kwa nini mnajishughulisha na kile ambacho wadhalimu hufanya kama watu wazee? Kwa nini mnaiga njia za zamani za mambo ya kale? Maisha yenu yanapaswa kujaa haki, ukweli, na utakatifu; maisha yenu hayapaswi kupotoshwa katika umri mdogo hivyo, yakiwasababisha kuanguka kuzimuni. Je, hamhisi kwamba hili ni la kusikitisha sana? Je, hamhisi kwamba hili silo haki kwenu sana?

Nyinyi nyote mnapaswa kufanya kazi yenu sahihi kabisa na kuidhabihu juu ya madhabahu Yangu kama dhabihu bora zaidi, za kipekee ambazo mnanipa. Nyote mnapaswa kusimama imara katika msimamo wenu wenyewe na msipeperushwe peperushwe na kila upepo mwanana kama mawingu angani. Mnafanya kazi kwa bidii nusu ya maisha yenu, basi kwa nini msitafute hatima mnapaswa kuwa nayo? Mnafanya kazi kwa bidii kwa muda wa nusu ya maisha ilhali mnawaacha wazazi wenu walio kama nguruwe na mbwa kukokota ukweli na umuhimu wa maisha yenu binafsi ndani ya kaburi. Je, huhisi kwamba huu ni udhalimu mkubwa dhidi yako? Je, huhisi kuwa kuishi maisha kwa njia hii ni kusiko na maana kabisa? Kutafuta ukweli na njia sahihi kwa njia hii mwishowe kutasababisha matatizo ili kuwa majirani ni wa wasiwasi na familia nzima haina furaha, na hupata misiba ya mauti—je, si wewe kuwa hivi ni maisha yasiyo na maana kabisa? Maisha ya nani yanaweza kuwa na bahati zaidi kuliko yako, na maisha ya nani yanaweza kuwa ya mzaha zaidi kuliko yako? Kunitafuta kwako si kwa ajili ya kupata furaha Yangu na kwa maneno ya faraja kwako? Lakini baada ya wewe kukimbia kimbia kwa nusu ya maisha na kisha kunichokoza mpaka Ninapojawa na hasira na kukupuuza au kutokusifu, basi si maisha yako yote ni bure? Na ungewezaje kuthubutu kwenda kuona roho za wale watakatifu katika enzi zote ambao wameondolewa toharani? Wewe hunijali na hatimaye unasababisha msiba wa mauti—ingekuwa bora zaidi kutumia fursa hii na kuwa na safari ya furaha kuvuka bahari kubwa mno na kisha kusikiza “utoaji” Wangu. Niliwaambia zamani kwamba wewe leo, kama usiyejali ilhali hutaki kuondoka, hatimaye ungeingizwa na kumezwa na mawimbi yaliyoinuliwa na Mimi. Je, kwa kweli mnaweza kujilinda wenyewe? Je, una imani kwamba mbinu yako ya sasa ya ukimbizaji itahakikisha kuwa unakamilishwa? Je, moyo wako si mgumu sana? Kufuata kwa aina hii, ukimbizaji wa aina hii, maisha ya aina hii, na tabia ya aina hii—jinsi gani vingeweza kupata sifa Yangu?

Tanbihi:

a. Hadithi ya ndege wa Hanhao inafanana sana na hekaya ya Aesop ya mchwa na panzi. Ndege wa Hanhao hupenda zaidi kulala kuliko kujenga kiota wakati hali ya hewa ni ya vuguvugu, licha ya onyo la marudio kutoka kwa jirani wake, ndege wa jamii ya kunguru. Wakati majira ya baridi hufika, ndege huyo huganda hadi kifo.

Unapaswa Kujua Namna Ambavyo Binadamu Wote Wameendelea Hadi Siku ya Leo

Kazi yote ya miaka 6,000 imebadilika kwa utaratibu kuambatana na nyakati. Mabadiliko katika kazi hii yamefanyika kulingana na hali za ulimwengu mzima. Kazi ya usimamizi ya Mungu imebadilika tu kwa utaratibu kulingana na mitindo ya kimaendeleo ya binadamu kwa ujumla; haikuwa imepangwa tayari mwanzoni mwa uumbaji. Kabla ya ulimwengu kuumbwa, au punde tu baada ya kuumbwa kwake, Yehova bado hakuwa amepanga hatua ya kwanza ya kazi, ile ya sheria; hatua ya pili ya kazi, ile ya neema; au hatua ya tatu ya kazi, ile ya kushinda, ambapo Angefanya kazi kwanza miongoni mwa kundi la watu—baadhi ya vizazi vya Moabu, na kupitia hili Angeweza kuushinda ulimwengu mzima. Hakuyaongea maneno haya baada ya kuumba ulimwengu; Hakuyaongea maneno haya baada ya Moabu, wala hata kabla ya Lutu. Kazi Yake yote ilifanywa bila kupangwa. Hivi ndivyo hasa kazi Yake nzima kwa usimamizi wa miaka elfu sita imeendelea; kwa vyovyote vile, kabla kuumba dunia, Hakuwa ameandika mpango kama huo kwa mtindo wa kitu kama “Chati ya Muhtasari wa Maendeleo ya Binadamu.” Katika kazi ya Mungu, Anaonyesha moja kwa moja kile Alichu; Hapigi bongo kuunda mpango. Bila shaka, manabii wengi wameongea unabii mwingi, lakini bado haiwezi kusemekana kwamba kazi ya Mungu siku zote imekuwa ya upangaji mpango dhahiri; unabii ulitolewa kulingana na kazi halisi ya Mungu. Kazi Zake zote ni kazi halisi zaidi. Hufanya kazi Yake kufutana na maendeleo ya kila enzi, na inazingatia jinsi mambao yanabadilika. Kwake Yeye, kutekeleza kazi ni sawa na kutoa dawa kutibu ugonjwa; Akiwa anafanya kazi Yake, Anaangalia na kuendelea na kazi Yake kulingana na kile Alichoon. Katika kila hatua ya kazi Yake, Anaweza kuonyesha hekima Yake ya kutosha na kuelezea uwezo Wake wa kutosha; Anafichua hekima Yake ya kutosha na mamlaka Yake ya kutosha kulingana na kazi ya enzi hiyo husika na kuruhusu yeyote kati ya watu waliorudishwa na Yeye wakati wa enzi hizo kuweza kuiona tabia Yake nzima. Anawaruzuku watu na kutekeleza kazi Anayofaa kufanya kulingana na kazi ambayo lazima ifanywe katika kila enzi; Anawaruzuku watu kulingana na kiwango ambacho Shetani amewapotosha. Ilikuwa namna hii wakati Yehova aliwaumba Adamu na Hawa mwanzoni ili kuwaruhusu kumdhihirisha Mungu katika dunia na kuwa na mashahidi wa Mungu miongoni mwa uumbaji, lakini Hawa alitenda dhambi baada ya kujaribiwa na nyoka; Adamu alifanya vivyo hivyo, na kwa pamoja wakiwa kwenye bustani wakalila tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Na hivyo basi, Yehova alikuwa na kazi ya ziada ya kutenda miongoni mwao. Aliuona

uchi wao na kuifunika mili yao kwa nguo ziliyotengenezwa kutoka kwa ngozi za wanyama. Kufuatia haya, Alimwambia Adamu “Kwa sababu umesikiliza sauti ya mkeo, na umekula kutoka kwa mti ule, ambao Nilikuamuru, nikisema, usile kutoka kwa mti huo: udongo umelaaniwa kwa sababu yako ... mpaka urudi udongoni, kwani ulitolewa hapo: kwa kuwa wewe ni mavumbi, na utarudi mavumbini.” Kwa mwanamke Akasema, “Nitazidisha sana sikitiko lako na kupata kwako watoto; utazaa watoto kwa sikitiko; na ashiki yako itakuwa kwa mume wako, na atatawala juu yako.” Kuanzia hapo kuendelea, aliwafukuza kutoka kwenye Bustani ya Edeni na kuwafanya waishi nje ya bustani, kama vile binadamu wa kisasa afanyavyo duniani. Mungu alipomwumba mwanadamu mwanzoni kabisa, Hakupanga kumfanya binadamu ajaribiwe na nyoka baada ya kuumbwa na kisha kuwalaani binadamu na nyoka. Kwa hakika hakuwa na mpango wa aina hii; ilikuwa tu maendeleo ya mambo yaliyompa kazi hii mpya miongoni mwa uumbaji Wake. Baada ya Yehova kutekeleza kazi Yake miongoni mwa Adamu na Hawa kwenye ardhi, binadamu waliendelea kuimarika kwa miaka elfu kadhaa mpaka “Yehova aliona kwamba uovu wa mwanadamu ulikuwa mkubwa ulimwenguni, na kuwa kila wazo la fikira za moyo wake lilikuwa ovu tu daima. Na Yehova akajuta kwamba alikuwa amemwumba mwanadamu ulimwenguni, na akawa na huzuni moyoni mwake. ... Lakini Nuhu alipata neema katika macho ya Yehova.” Wakati huu Yehova alikuwa na kazi mpya zaidi, kwa ajili binadamu Aliowaumba walikuwa wamezidisha dhambi baada ya kujaribiwa na nyoka. Kwa mujibu wa hali hizi, Yehova aliichagua familia ya Nuhu kutoka miongoni mwa watu hawa na kuwanusuru, na kutekeleza kazi Yake ya kuuangamiza ulimwengu kwa gharika. Binadamu wameendelea kukua kwa njia hii mpaka siku ya leo, wakiendelea kupotoka kwa kukithiri, na wakati maendeleo ya binadamu yafikapo kilele, utakuwa ndio mwisho wa binadamu. Kuanzia mwanzo kabisa hadi mwisho wa ulimwengu, ukweli wa ndani wa kazi Yake siku zote umekuwa hivi. Hii ni sawa na namna ambavyo watu watakavyoainishwa kulingana na aina yao; hii ni mbali na hali ya kwamba kila mtu anayeamuliwa kabla kwa kikundi fulani; bali kila mtu anaainishwa polepole baada ya kupitia mchakato wa maendeleo. Mwishowe, yeyote ambaye hawezi kuokolewa kwa ukamilifu atarudishwa kwa mababu zake. Hamna kati ya kazi za Mungu miongoni mwa binadamu iliyokuwa tayari imetayarishwa wakati wa uumbaji wa ulimwengu; badala yake, ilikuwa ni maendeleo ya mambo yaliyomruhusu Mungu kutekeleza kazi Yake hatua kwa hatua kwa uhalisia zaidi na kwa kimatendo zaidi miongoni mwa binadamu. Hivi ni kama ambavyo Yehova Mungu hakumwumba nyoka ili kumjaribu mwanamke. Haukuwa mpango Wake mahususi, wala halikuwa jambo ambalo Alikuwa ameliambia kimakusudi kabla; mtu anaweza kusema kwamba hili halikutarajiwa. Hivyo basi ilikuwa ni kwa sababu ya hili ndiyo Yehova aliwatimua Adamu na Hawa kutoka kwenye Bustani ya Edeni na kuapa kutowahi kumwumba binadamu tena. Lakini hekima ya Mungu inagunduliwa tu na watu kwenye msingi huu, kama tu ile hoja Niliyotaja awali: “Hekima Yangu hutumika kutokana na njama za Shetani.” Haikujalisha ni vipi ambavyo

binadamu walizidi kupotoka au vipi nyoka alivyowajaribu, Yehova bado alikuwa na hekima Yake; kwa hivyo, Amekuwa Akijihusisha katika kazi mpya tangu Alipoumba ulimwengu, na hamna hatua zozote za kazi hii zimewahi kurudiwa. Shetani ameendelea kutekeleza njama zake; binadamu wamekuwa wakipotoshwa siku zote na Shetani, na Yehova Mungu pia ameendelea kutekeleza kazi Yake ya hekima siku zote. Hajawahi kushindwa, na Hajawahi kusita kufanya kazi Yake kuanzia uumbaji wa ulimwengu mpaka sasa. Baada ya binadamu kupotoshwa na Shetani, Aliendelea siku zote kufanya kazi miongoni mwa watu ili kumshinda adui Wake anayewapotosha binadamu. Vita hivi vitaendelea kuanzia mwanzo hadi mwisho wa ulimwengu. Kwa kufanya kazi hii yote, Hajaruhusu tu binadamu, ambao wamepotoshwa na Shetani, kupokea wokovu Wake mkubwa, lakini pia amewaruhusu kuiona hekima Yake, uweza na mamlaka, na hatimaye Atawaruhusu binadamu kuiona tabia Yake ya haki—huku Akiwaadhibu waovu na kuwatuza wema. Amepambana na Shetani hadi siku hii ya leo na Hajawahi kushindwa, kwani Yeye ni Mungu mwenye hekima, na hekima Yake hutumika kutokana na njama za Shetani. Na kwa hivyo mbali na kufanya tu kila kitu mbinguni kitii mamlaka Yake; pia Hufanya kila kitu duniani kipumzike chini ya kigonda Chake na pia, Huwafanya wale waovu wanaoshambulia na kunyanyasa binadamu wajipate katika kuadibu Kwake. Matokeo yote ya kazi yanaletwa kutokana na hekima Yake. Alikuwa hajawahi kufichua hekima Yake kabla ya uwepo wa binadamu, kwani Hakuwa na maadui kule mbinguni, juu ya dunia, au kwenye ulimwengu kwa ujumla, na hakukuwa na nguvu za giza zilizoshambulia chochote katika maumbile. Baada ya malaika mkuu kumsaliti, Aliwaumba binadamu kwenye dunia, na ilikuwa ni kwa sababu ya binadamu ndiyo Alianza rasmi vita Vyake vya milenia nzima dhidi ya Shetani, malaika mkuu, vita ambavyo vilizidi kushamiri kwa kila hatua iliyopigwa. Uweza Wake na hekima vinapatikana katika kila mojawapo ya awamu hizi. Ni katika muda huu tu ndipo kila kitu kule mbinguni na duniani huweza kushuhudia hekima ya Mungu, uweza Wake, na hasa uhalisi wa Mungu. Angali anatekeleza kazi Yake kwa njia ile ya kihalisi leo; aidha, Anapoendelea kutekeleza kazi Yake anafichua pia uweza Wake na hekima Yake; Anawaruhusu kuona ule ukweli wa ndani katika kila hatua ya kazi, kuona hasa ni vipi mnaweza kuelezea uweza wa Mungu na hasa ni vipi mnavyoweza kuelezea uhalisia wa Mungu.

Kuhusu Yuda kumsaliti Yesu, watu wengine hushangaa: Je, hili halikuwa liamuliwa kabla ya uumbaji wa ulimwengu? Kwa hakika, Roho Mtakatifu alikuwa amepanga haya kulingana na uhalisi wakati huo. Ilitukia tu kwamba kulikuwepo mtu kwa jina la Yuda ambaye siku zote angebadhiri fedha. Hivyo basi alichaguliwa kutekeleza wajibu huu na kuwa mwenye huduma katika njia hii. Huu ni mfano halisi wa kutumia rasilimali za mahali palepale. Yesu hakujua hili kwanza; Alilijua hili tu Yuda alipolifichuliwa baadaye. Kama mtu mwingine angeweza kutekeleza wajibu huu, basi mtu mwingine angeweza kufanya hivi badala ya Yuda. Kile

ambacho kiliamuliwa awali kiliweza hasa kufanywa wakati mmoja na Roho Mtakatifu. Kazi ya Roho Mtakatifu siku zote inafanywa kwa hiari; wakati wowote Anapopanga kazi Yake, Roho Mtakatifu ataitekeleza. Kwa nini sikuzote Nasema kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ni ya uhalisi? Kwamba siku zote ni mpya na haijawahi kuwa zee, na siku zote inakuwa na uhai zaidi? Kazi Yake bado haikuwa imepangwa wakati ulimwengu ulipoumbwa; hivi sivyo kamwe ilivyofanyika! Kila hatua ya kazi hufikia athari yake bora kwa wakati wake mwafaka, nazo haziingiliani kati. Kunao wakati mwingi ambapo mipango katika akili zako hazilingani kamwe na kazi ya hivi punde ya Roho Mtakatifu. Kazi Yake si rahisi kama wanavyofikiria watu, wala si ngumu kama watu wengi wanavyofikiria; inajumuisha kuwaruzuku watu wakati wowote na mahali popote kulingana na mahitaji yao ya sasa. Hakuna aliye wazi zaidi kuhusu kiini halisi cha watu kama Yeye, na ni kwa sababu hii mahususi ndiposa hakuna kinachoweza kufaa mahitaji ya kihalisi ya watu kama vile ambavyo kazi Yake inavyofanya. Hivyo basi, kutoka katika mtazamo wa kibinadamu, kazi Yake ilipangiwa milenia kadha mbele. Anavyofanya kazi miongoni mwenu sasa, kulingana na hali yenu, Yeye pia Anafanya kazi na kuongea wakati wowote na mahali popote. Wakati watu wako katika hali fulani, Yeye huongea maneno hayo ambayo hasa ndiyo wanayohitaji ndani yao. Ni kama hatua ya kwanza ya kazi Yake, nyakati za kuadibu. Baada ya nyakati za kuadibu, watu walionyesha tabia fulani, walikuwa na mienendo ya kuasi katika njia fulani, hali fulani nzuri ziliibuka, hali fulani hasi pia ziliibuka, na mipaka ya juu ya uhasi huu ikafikia kiwango fulani. Mungu alifanya kazi Yake kwa msingi wa mambo haya yote, na hivyo basi Alichukua haya yote ili kuweza kutimiza athari bora zaidi kwa ajili ya kazi Yake. Anatekeleza tu kazi Yake ya kuruzuku miongoni mwa watu kulingana na hali zao za sasa. Yeye Hutekeleza kila hatua ya kazi Yake kulingana na hali halisi za watu. Viumbe wote wamo mikononi Mwake; Angekosa kuujua? Kwa mujibu wa hali za watu, Mungu hutekeleza hatua inayofuata ya kazi inayofaa kufanywa, wakati na mahali popote. Kazi hii haikupangwa maelfu ya miaka kabla; hii ni dhana ya kibinadamu tu! Yeye hufanya kazi huku akiangalia athari za kazi Yake, na kazi Yake inaendelea kuwa ya kina na kukua; Anapoendelea kuangalia matokeo ya kazi Yake, Anatekeleza hatua inayofuata ya kazi Yake. Yeye hutumia mambo mengi ili kuingia kwenye mpito hatua kwa hatua na kufanya kazi Yake mpya kuonekana na watu baada ya muda. Aina hii ya kazi inaweza kuruzuku mahitaji ya watu, kwani Mungu anawajua watu vizuri mno. Hivi ndivyo Anavyotekeleza kazi Yake kutoka mbinguni. Vilevile, Mungu mwenye mwili anafanya kazi Yake kwa njia iyo hiyo, Akipangilia kulingana na uhalisi na kufanya kazi miongoni mwa binadamu. Hakuna yoyote kati ya kazi Yake iliyopangwa kabla ya ulimwengu kuumbwa, wala kupangwa kwa umakinifu kabla ya wakati. Miaka elfu mbili baada ya ulimwengu kuumbwa, Yehova aliona binadamu walikuwa wamepotoka sana kiasi cha kwamba Alikitumia kinywa cha nabii Isaya kutabiri kwamba baada ya Enzi ya Sheria kukamilika, Angetekeleza kazi Yake ya kukomboa binadamu katika Enzi ya Neema. Huu ulikuwa mpango

wa Yehova, bila shaka, lakini mpango huu pia kufanywa kulingana na hali ambazo Aliangalia wakati huo; bila shaka Yeye hakuufikiria mara moja baada ya kumwumba Adamu. Isaya alitabiri tu, lakini Yehova hakuwa amefanya matayarisho ya mapema ya kazi hii wakati wa Enzi ya Sheria; badala yake, Alianza kazi hii katika mwanzo wa Enzi ya Neema, wakati mjumbe alipojitokeza katika ndoto ya Yusufu na kumpa yeye nuru, akimwambia kwamba Mungu angekuwa mwili, na hivyo kazi Yake ya kupata mwili ikaanza. Kama watu wanavyofikiria Mungu hakujitayarishia kazi Yake ya kuwa mwili baada ya kuumba ulimwengu; jambo hili liliamuliwa tu kulingana na kiwango cha maendeleo ya binadamu na hadhi ya vita Vyake na Shetani.

Mungu anapokuja kuwa mwili, Roho Wake anamshukia binadamu; kwa maneno mengine, Roho wa Mungu anauvaa mwili. Anafanya kazi Yake duniani, na badala ya kuleta naye hatua mbalimbali zilizozuiliwa, kazi hii haina mipaka kamwe. Kazi ambayo Roho Mtakatifu hufanya katika mwili bado inaamuliwa na athari ya kazi Yake, na Yeye hutumia mambo haya kuamua urefu wa muda ambao Atafanya kazi akiwa katika mwili. Roho Mtakatifu hufichua moja kwa moja kila hatua ya kazi Yake; Yeye huchunguza kazi Yake anapozidi kuendelea; si jambo la kimwujiza kiasi cha kupanua ile mipaka ya kufikiriwa na binadamu. Hii ni kama kazi ya Yehova katika kuumba mbingu na nchi na vitu vyote; Aliweza kupanga na kufanya kazi wakati huo huo. Alitenga nuru kutoka kwenye giza, na asubuhi pamoja na jioni vyote vikawepo—hii ilichukua siku moja. Siku ya pili Aliumba mbingu, ambayo pia ilichukua siku moja na kisha Akaiumba nchi, bahari na viumbe vilivyojaa ndani, pia ikichukua siku nyingine moja. Hili liliendelea hivyo hadi siku ya sita, wakati Mungu alipomwumba binadamu na kumwacha asimamie viumbe hivi vyote juu ya nchi, mpaka siku ya saba, Alipokuwa amemaliza kuumba viumbe vyote, na akapumzika. Mungu alibariki siku ya saba na kuitenga kuwa siku takatifu. Aliiamulia siku hii takatifu baada ya kuviumba viumbe vyote, na wala si kabla ya kuviumba. Kazi hii pia ilitekelezwa kwa hiari; kabla ya kuviumba viumbe vyote, Hakuamua kuumba ulimwengu kwa siku sita na kupumzika siku ya saba; ukweli hauko hivi hata kidogo. Hakusema hili, wala Hakupanga hili. Kwa vyovyote vile Hakusema kwamba uumbaji wa viumbe vyote ungekamilishwa katika siku ya sita na kwamba Angepumzika katika siku ya saba; badala yake, Aliumba kulingana na kile kilichokuwa kikionekana kizuri Kwake. Punde Alipomaliza kuumba kila kitu, tayari ilikuwa ni siku ya sita. Kama ingekuwa ni siku ya tano Alipomaliza kuumba kila kitu, Angepangilia basi siku ya sita kuwa siku takatifu; hata hivyo, Alimaliza kuumba kila kitu katika siku ya sita, na hivyo basi siku ya saba ikawa siku takatifu, ambayo imepitishwa hadi siku ya leo. Hivyo basi, kazi Yake ya sasa inatekelezwa kwa njia ii hii. Yeye huongea na kuwaruzuku kulingana na hali zenu. Yaani, Roho huongea na kufanya kazi kulingana na hali za watu; Roho huangalia kila kitu na kufanya kazi wakati wowote na mahali popote. Kile Ninachofanya, kwa

mfano, kuwawekea na kuwapa bila kiwazo ni kile mnachohitaji. Kwa hivyo hakuna kazi Yangu iliyo tofauti na uhalisi; yote ni halisi, kwani nyinyi nyote mnajua ya kwamba “Roho wa Mungu hulinda vyote.” Kama haya yote yalikuwa yameamuliwa kabla ya wakati, huoni kwamba mambo yangekuwa yamekwisha amuliwa? Unafikiri kwamba Mungu alifanya kazi kwa milenia sita nzima na kisha kuamulia kabla binadamu kama waasi, wapingaji, waongo na wadanganyifu, kama kuwa na upotovu wa mwili, tabia za kishetani, ashiki za macho na kujihusisha kwao kwa mambo yasiyofaa. Haya yote hayakupangwa na Mungu, lakini yalitokana na upotoshaji wa Shetani. Baadhi watasema, “Shetani naye hakuwa ndani ya mfumbato wa Mungu? Mungu alikuwa amepanga awali kwamba Shetani angepotosha binadamu kwa njia hii, na baada ya hapo Akatekeleza kazi Yake miongoni mwa binadamu.” Je, Mungu kwa kweli angepanga awali Shetani kuwapotosha binadamu? Anayo hamu mno ya kuwaruhusu binadamu kuishi maisha ya kawaida na kibinadamu; Angenyanyasa maisha ya binadamu? Kama hali ni hivyo, kumshinda Shetani na kuokoa binadamu si kungekuwa jitihada za bure bilashi? Je, uasi wa binadamu ungeamuliwaje kabla? Ulitokana na kunyanyaswa na Shetani kwa hali halisi; ungepangwa vipi awali na Mungu? Shetani aliye ndani ya mfumbato wa Mungu ambaye mnamwelewa na Shetani ndani ya mfumbato wa Mungu ambaye Ninamzungumzia ni tofauti sana. Kulingana na kauli zenu kwamba “Mungu ni mwenyezi, na Shetani yumo mikononi Mwake,” Shetani asingemsaliti Yeye. Je, wewe hujasema kwamba Mungu ni mwenyezi? Maarifa yenu ni ya kidhahania mno na hayaambatani na uhalisi; mwanadamu kamwe hawezi kuelewa fikira za Mungu, wala mwanadamu hawezi kamwe kuelewa busara ya Mungu! Mungu ni mwenyezi; huu si uwongo kamwe. Malaika mkuu alimsaliti Mungu kwa sababu Mungu alimpa sehemu ya mamlaka awali. Bila shaka, tukio hili halikutarajiwa, kama vile Hawa kushindwa na jaribio la nyoka. Hata hivyo, bila kujali ni vipi ambavyo Shetani hutekeleza usaliti wake, tofauti na Mungu, yeye si mwenyezi. Kama vile mlivyosema, Shetani ni mwenye nguvu; haijalishi ni nini atakachofanya, mamlaka ya Mungu humshinda siku zote. Hii ndiyo maana ya kweli katika ule msemu “Mungu ni mwenyezi, na Shetani yumo mikononi Mwake.” Hivyo basi, vita Vyake na Shetani lazima vitekelezwe hatua moja baada ya nyingine; aidha, Yeye hupanga kazi Yake katika kuitikia ujanja wa Shetani. Hivi ni kusema, kulingana na enzi, Anawaokoa watu na kufichua hekima na uweza Wake. Vilevile, kazi za siku za mwisho haikuamuliwa mapema, kabla ya Enzi ya Neema; kuamuliwa kabla hakufanywi kwa njia ya kawaida kama hii: mwanzo, kwa kuifanya tabia ya nje ya binadamu ibadilike; pili, kumweka chini ya uongozi binadamu apokee adabu na majaribio yake; tatu, kusababisha binadamu kupitia jaribio la kifo; nne, kumfanya binadamu apitie nyakati za kumpenda Mungu na aonyeshe uamuzi wa kiumbe kilichoumbwa; tano, kumruhusu binadamu kuweza kuona mapenzi ya Mungu na kumjua Yeye kikamilifu; na hatimaye, kisha kumkamilisha binadamu. Hakupanga mambo haya yote wakati wa Enzi ya Neema; badala yake, Alianza kuyapanga katika enzi ya sasa. Shetani yumo kazini, kama vile alivyo Mungu. Shetani

huonyesha tabia yake potovu, huku naye Mungu huongea moja kwa moja na kufichua baadhi ya mambo muhimu. Hii ndiyo kazi inayofanywa leo, na kanuni ii hii ya kufanya kazi ilitumika zamani, baada ya ulimwengu kuumbwa.

Kwanza Mungu aliwaumba Adamu na Hawa, na pia Alimwumba nyoka. Miongoni mwa vitu vyote, nyoka ndiye aliyekuwa mwenye sumu nyingi sana; mwili wake ulikuwa na sumu, na Shetani aliitumia sumu hii ili kufaidika naye. Ni nyoka aliyemjaribu Hawa hadi akatenda dhambi. Adamu alitenda dhambi baada ya Hawa kutenda, na wawili hawa kisha waliweza kutofautisha kati ya mema na maovu. Kama Yehova angejua kwamba nyoka angemjaribu Hawa, na kwamba Hawa angemjaribu Adamu, kwa nini Akawaweka wote pale ndani ya bustani? Kama Aliweza kutabiri mambo haya kwa nini Akamwumba nyoka na kumweka ndani ya Bustani ya Edeni? Kwa nini Bustani ya Edeni ilikuwa na tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya? Aliniuia wao walile hilo tunda? Yehova alipokuja, Adamu wala Hawa hawakuthubutu kumkabili Yeye, na ulikuwa tu wakati huu ambapo Yehova alijua kwamba walikuwa wamelila tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya na kushikwa katika ujanja wa yule nyoka. Hatimaye Alimlaani nyoka, na Akamlaani Adamu na Hawa pia. Wakati hao wawili walilila tunda lile la mti, Yehova hakujua kabisa kwamba walikuwa wakifanya hivyo. Binadamu walipotoka hadi kufikia kiwango cha kuwa na uovu na uasherati wa kimapenzi, hadi kufikia hatua ambayo mambo yote waliyokuwa nayo katika mioyo yao yalikuwa maovu na yasiyo ya haki; yote yalikuwa machafu. Yehova hivyo basi alijutia kuumba binadamu. Baadaye Alitekeleza kazi Yake ya kuharibu ulimwengu kwa gharika, ambayo Nuhu na watoto wake wa kiume walinusurika. Baadhi ya mambo kwa hakika hayajaendelea na kuwa ya mwujiza kama vile watu wanavyoweza kufikiria. Baadhi wanauliza: “Kwa sababu Mungu alijua malaika mkuu angemsaliti Yeye, kwa nini Alimwumba?” Huu ndio ukweli: Wakati dunia haikuwepo bado, malaika mkuu ndiye aliyekuwa malaika mkuu zaidi mbinguni. Alikuwa na mamlaka juu ya malaika wote kule mbinguni; haya ndiyo yaliyokuwa mamlaka ambayo Mungu alimpa. Kando na Mungu, yeye ndiye aliyekuwa malaika mkubwa zaidi mbinguni. Wakati Mungu alipoumba binadamu baadaye, malaika mkuu alitekeleza usaliti mkuu zaidi dhidi ya Mungu duniani. Nasema kwamba alimsaliti Mungu kwa sababu alitaka kuwasimamia binadamu na kuzidi mamlaka ya Mungu. Ni malaika mkuu ambaye alimjaribu Hawa hadi akatenda dhambi; alifanya hivyo kwa sababu alipenda kuanzisha ufalme wake duniani na kuwafanya binadamu wamsaliti Mungu na kumtii yeye badala yake. Aliona kwamba kulikuwa na vitu vingi ambavyo vilimtii; malaika walimtii sawa na vile ambavyo watu wa dunia walivyomtii. Ndege na wanyama, miti, misitu, milima, mito na vitu vyote vilivyo duniani vilikuwa chini ya utunzaji wa binadamu—yaani, Adamu na Hawa—huku nao Adamu na Hawa wakimtii. Malaika mkuu hivyo basi alitamani kuzidi mamlaka ya Mungu na kumsaliti Mungu. Baadaye aliwaongoza malaika wengi kumsaliti Mungu, ambao baadaye walikuja kuwa

pepo wachafu mbalimbali. Je, maendeleo ya binadamu hadi siku ya leo hayajasababishwa na upotovu wa malaika mkuu? Binadamu wako tu namna walivyo leo kwa sababu malaika mkuu alimsaliti Mungu na kuwapotosha binadamu. Kazi hii ya hatua kwa hatua haiko karibu kuwa ya dhahania na rahisi kama vile watu wanavyofikiria hata kidogo. Shetani alitekeleza usaliti wake kwa sababu fulani, ilhali watu hawawezi kufahamu kitu rahisi kama hicho. Kwa nini Mungu akaziumba mbingu na dunia na vitu vyote, na pia kumwumba Shetani? Kwa sababu Mungu anamdharau Shetani sana, naye Shetani ni adui Wake, kwa nini akamwumba Shetani? Kwa kumwumba Shetani, hakuwa Anamwumba adui? Mungu kwa hakika hakuumba adui; badala yake, Alimwumba malaika, na baadaye malaika akamsaliti Yeye. Hadhi yake ilikuwa kubwa mno kiasi cha kwamba alitaka kumsaliti Mungu. Mtu anaweza kusema kwamba hii ilikuwa ni sadfa, lakini ulikuwa pia mwelekeo usioepukika. Ni sawa na vile ambavyo mtu bila kuepuka atakufa akiwa na umri fulani; mambo yameendelea tayari hadi kwa hatua fulani. Kunao hata wapumbavu wengine wanaosema: “Kwa sababu Shetani ni adui Yako, kwa nini Ukamwumba? Kwani hukujua kuwa malaika huyu mkuu angekusaliti Wewe? Kwani Huwezi kukazia macho kutoka kwa milele hadi milele? Kwani Wewe huijui asili yake? Kwa sababu Ulijua waziwazi kuwa angekusaliti Wewe, basi kwa nini Ukamfanya kuwa malaika mkuu? Hata kama mtu atapuza suala la usaliti wake, bado aliwaongoza malaika wengi sana na akashuka hadi kwa ulimwengu wa binadamu wenye kufa ili kuwapotosha binadamu; hadi siku ya leo Umeshindwa kukamilisha mpango Wako wa usimamizi wa miaka elfu sita.” Je, maneno haya ni sahihi? Unapofikiria kwa njia hii, hujiweki katika matatizo mengi zaidi kuliko yanayohitajika? Wengine bado husema: Kama Shetani asingewapotosha binadamu hadi siku ya leo, Mungu asingewaokoa binadamu kwa njia hii. Katika mfano huu, hekima na uweza wa Mungu vyote vingekuwa havionekani; hekima Yake ingejionyesha wapi? Hivyo basi Mungu alikiumba kizazi cha binadamu kwa minajili ya Shetani; katika siku za baadaye, Mungu angefichua uweza Wake—vinginevyo, binadamu angewezaje kugundua hekima ya Mungu? Kama binadamu asingempinga Yeye na kumwasi Yeye, isingehitajika kwa vitendo Vyake kujionyesha. Kama viumbe wote wangemwabudu Yeye na kumtii Yeye, Asingekuwa na kazi ya kufanya. Hali hii ni mbali zaidi na uhalisi wa mambo, kwani hakuna chochote kichafu kuhusu Mungu, na hivyo basi Hawezi kuumba uchafu. Yeye hufichua vitendo Vyake sasa ili kuweza tu kuwashinda kabisa adui Zake, ili kuokoa binadamu, ambao Aliwaumba, ili kuyashinda mapepo na Shetani, ambao wanamchukia, wanamsaliti na wanampinga, ambao walikuwa chini ya utawala Wake na alikuwa Wake mwanzoni kabisa; Anataka kuwashinda hawa mapepo na katika kufanya hivyo kuufichua uweza Wake kwa vitu vyote. Binadamu na vitu vyote vilivyomo duniani sasa hivi vinamilikiwa na Shetani na katika umiliki wa waovu. Mungu anataka kuvifichua vitendo Vyake kwa vitu vyote ili watu waweze kumjua Yeye, na hivyo kuishia kumshinda Shetani na kuwaangamiza kabisa adui Zake. Uzima wa kazi hii unakamilishwa kupitia kufichua matendo Yake. Viumbe

Vyake vyote vimemilikiwa na Shetani, na hivyo basi Angependa kuufichua uweza Wake kwa viumbe hivyo, na hivyo kumshinda Shetani. Kama Shetani asingekuwepo, Asingehitaji kuyafichua matendo Yake. Kama usingekuwa usumbufu wa Shetani, Angewaumba binadamu na kuwaongoza kuishi katika Bustani ya Edeni. Kwa nini Hakuwahi kufichua vitendo Vyake vyote kwa malaika au malaika mkuu kabla ya kusalitiwa na Shetani? Kama malaika na malaika mkuu wanalimjua Yeye, na pia kumtii Yeye pale mwanzoni, basi Asingetekeleza vile vitendo vya kazi visivyo na maana. Kwa sababu ya uwepo wa Shetani na mapepo, watu humpinga na wanajazwa hadi pomoni na tabia ya uasi, na hivyo basi Mungu angependa kufichua vitendo Vyake. Kwa sababu Angependa kupigana vita na Shetani, lazima Atumie mamlaka Yake kumshinda Shetani na kutumia vitendo Vyake vyote kumshinda Shetani; kwa njia hii, kazi Yake ya wokovu Anayotekeleza miongoni mwa binadamu itawafanya watu waone hekima na uweza Wake. Kazi anayofanya Mungu leo ni yenye maana na haifanani hata kidogo kile watu wengine husema: “Je, kazi hii Unayofanya haihitilafiani? Je, hujisumbui tu na huu mfululizo wa kazi? Ulimwumba Shetani, kisha ukamruhusu Akakusaliti na kukupinga Wewe. Uliwaumba binadamu, na kisha ukawakabidhi kwa Shetani, na Ukaruhusu Adamu na Hawa wajaribiwe. Kwa sababu uliyafanya mambo haya yote kimakusudi, kwa nini Unawachukia binadamu? Kwa nini Unamchukia Shetani? Mambo haya si ya kujitungia Mwenyewe? Kuna nini cha Wewe kuchukia?” Watu wengi wa kipumbavu watasema hayo. Wanatamani kumpenda Mungu, lakini mioyoni mwao wanalalamika kumhusu Mungu—ukinzani kweli! Wewe huelewi ukweli, unazo fikira nyingi sana za kimiujiza, na pia unadai kwamba hili ni kosa la Mungu—wewe ni mpumbavu kweli! Ni wewe unayechezacheza na ukweli; si kosa la Mungu! Baadhi ya watu hata watalalamika na kulalamika: “Ni wewe uliyemwumba Shetani, na ni Wewe uliyemrusha Shetani hadi katika ulimwengu wa mwanadamu na uliyemkabidhi binadamu kwake. Binadamu wana tabia ya kishetani; badala ya kuwasamehe, Unawachukia sana kwa kiwango fulani. Mwanzoni Uliwapenda binadamu kwa kiwango fulani, na sasa Unawachukia sana binadamu. Ni Wewe unayewachukia sana na kuwapenda binadamu—maelezo ya haya ni yapi? Je, huu si ukinzani?” Bila kujali ni vipi mnavyoangalia suala hili, hili ndilo lililofanyika mbinguni; malaika mkuu alimsaliti Mungu kwa njia hii, nao binadamu wakapotoshwa kwa njia hii, na wakaendelea mpaka leo kwa njia hii. Bila kujali ni vipi mnavyolisema, hii ndiyo hadithi yote. Hata hivyo, lazima muelewe kwamba Mungu anaifanya kazi ya leo ili kuwaokoa nyinyi, na ili kumshinda Shetani.

Kwa sababu malaika hasa walikuwa wanyonge na hawakuwa na uwezo wowote, walikuwa mwenye kiburi wakati walipewa mamlaka, hasa malaika mkuu, ambaye hadhi yake ilikuwa ya juu zaidi kuliko ile ya malaika mwingine yeyote. Malaika mkuu alikuwa ndiye mfalme wa malaika wote. Aliwaongoza mamilioni ya malaika, na chini ya Yehova mamlaka yake yalizidi yale ya malaika yeyote mwingine. Alitaka kufanya hivi na vile, na kuwaongoza malaika hadi

ulimwenguni mwa binadamu ili kuutawala ulimwengu. Mungu alisema kwamba Yeye huutawala ulimwengu; malaika mkuu akasema kwamba ulimwengu ulikuwa wake wa kutawala, na kuanzia hapo akamsaliti Mungu. Mbinguni, Mungu alikuwa ameuumba ulimwengu mwingine. Malaika mkuu akataka kuutawala ulimwengu huu na pia kushuka chini kwenye ulimwengu wa binadamu. Je, Mungu angemruhusu kufanya hivi? Hivyo basi, Alimpiga malaika mkuu na kumtimua chini hadi katikati ya anga. Tangu hapo alipowapotosha binadamu, Mungu amefanya vita dhidi yake ili kuwaokoa binadamu; Ametumia milenia hizi sita kumshinda. Dhana yenu ya mwenyezi Mungu hailingani na kazi ambayo Mungu anatekeleza sasa; haifanyi kazi katika kutenda na ni ya upumbavu ajabu! Kwa hakika, Mungu alitangaza malaika mkuu kuwa adui Yake baada tu ya malaika mkuu kumsaliti Yeye. Ilikuwa kutokana tu na kusaliti kwake Mungu ndiposa aliwakandamiza binadamu baada ya kuwasili katika ulimwengu wa binadamu, na ilikuwa kwa sababu hii ndiposa binadamu waliendelea hivyo hadi kwa hatua hii. Kufuatia haya, Mungu alikula kiapo na Shetani: “Nitakushinda wewe na kuwaokoa binadamu, viumbe Wangu.” Shetani hakushawishika wakati wa mwanzo na akasema, “Ni nini kwa hakika unachoweza kunifanyia mimi? Wewe kweli unaweza kuniangusha hadi katikati ya anga? Wewe unaweza kwa kweli kunishinda mimi?” Baada ya Mungu kumwangusha hadi katikati ya anga, Hakumtilia maanani tena na kisha Alianza kuwaokoa binadamu na kufanya kazi Yake mwenyewe, licha ya usumbufu ulioendelea kutoka kwa Shetani. Kila kitu ambacho Shetani angeweza kufanya kilitokana na nguvu alizopewa na Mungu; alichukua vitu hivi pamoja naye hadi katikati ya anga na amevihifadhi hadi leo. Alipomwangusha malaika mkuu hadi katikati ya anga, Mungu alimwangusha hadi angani lakini hakuchukua mamlaka yake, na hivyo basi aliendelea kuwapotosha binadamu. Mungu, kwa upande mwingine, Alianza kuwaokoa binadamu, ambao Shetani alikuwa amewapotosha baada ya kuumbwa kwao. Mungu hakufichua vitendo Vyake wakati akiwa mbinguni; hata hivyo, kabla ya kuiumba dunia, Aliwaruhusu watu katika ulimwengu Aliouumba mbinguni kuona vitendo Vyake na hivyo kuwaongoza watu juu mbinguni. Aliwapa hekima na akili, na kuwaongoza watu hao kuishi katika ulimwengu huo. Kiasili, hakuna kati yenu ambaye amewahi kusikia haya awali. Baadaye, baada ya Mungu kuumba binadamu, malaika mkuu alianza kuwapotosha binadamu; duniani, binadamu wote walikuwa katika machafuko. Ulikuwa ni wakati huu tu ambapo Alianza vita Vyake dhidi ya Shetani, na ulikuwa ni wakati huu tu ambapo watu waliona vitendo Vyake. Mwanzoni vitendo Vyake vilifichwa kutoka kwa binadamu. Baada ya Shetani kuangushwa hadi katikati ya anga, alijishughulisha na masuala yake, naye Mungu akajishughulisha Mwenyewe na kazi Yake binafsi, siku zote Akifanya vita dhidi ya Shetani, kila wakati mpaka siku za mwisho. Sasa ndio wakati ambapo Shetani anafaa kuangamizwa. Mwanzoni Mungu alimpa mamlaka, na baadaye Alimtimua hadi katikati ya anga, lakini Shetani alibaki mwasi. Baada ya hapo, aliwapotosha binadamu, lakini Mungu kwa hakika alikuwa ulimwenguni akiwasimamia binadamu. Mungu

hutumia usimamizi Wake wa watu kumshinda Shetani. Kwa kuwapotosha watu, Shetani hutamatisha majaaliwa ya watu na kuinyanyasa kazi ya Mungu. Kwa upande mwingine, kazi ya Mungu ndiyo wokovu wa binadamu. Ni hatua gani ya kazi ya Mungu mwenyewe ambayo hainuii kuwaokoa binadamu? Ni hatua gani hainuii kuwatakaswa watu, kuwafanya atende haki na kuwafanya kuishi kwa njia ambayo huunda taswira inayoweza kupendwa? Shetani, hata hivyo, hafanyi hivi. Yeye huwapotosha binadamu; siku zote anatekeleza kazi zake za kuwapotosha binadamu kote ulimwenguni. Bila shaka, Mungu pia hufanya kazi Yake mwenyewe. Hamtilii maanani Shetani. Haijalishi ni kiasi kipi cha mamlaka ambacho Shetani anacho, mamlaka yake bado yalitoka kwa Mungu; Mungu kwa hakika hakumpa mamlaka Yake yote tu, na hivyo basi haijalishi ni nini afanyacho, hawezi kuzidi Mungu na siku zote yuko mikononi mwa Mungu. Mungu hakufichua vitendo Vyake vyovyote akiwa mbinguni. Alimpa Shetani kiwango kidogo tu cha mamlaka ili kumruhusu kutekeleza udhibiti wake dhidi ya malaika. Hivyo basi, haijalishi kile anachofanya, hawezi kuzidi mamlaka ya Mungu kwa sababu mamlaka ambayo Mungu alimpa awali ni finyu. Huku Mungu akifanya kazi, Shetani hunyanyasa. Katika siku za mwisho, atamaliza unyanyasaji wake; vilevile, kazi ya Mungu itakamilika, na aina ya mtu ambaye Mungu angependa kumkamilisha atakuwa amekamilika. Mungu huwaelekeza watu kwa njia nzuri; maisha Yake ni maji yenye uzima, yasiyopimika na yasiyo na mipaka. Shetani amempotosha binadamu hadi kiwango fulani; hatimaye, yale maji hai ya uzima yatamkamilisha binadamu, na haitawezekana kwa Shetani kuingilia kati na kutekeleza kazi yake. Hivyo basi, Mungu ataweza kuwapata kabisa watu wake. Shetani angali anakataa kukubali haya sasa; siku zote hupambana na Mungu, lakini Mungu hamtilii maanani. Amesema, Nitakuwa mshindi dhidi ya nguvu zote za giza za Shetani na dhidi ya ushawishi wote wa giza. Hii ndiyo kazi ambayo lazima ifanywe katika mwili, na ndiyo pia maana ya kupata mwili kwa Yesu Kristo. Ni kukamilisha hatua ya kazi ya kumshinda Shetani katika siku za mwisho, kuondoa vitu vyote vinavyomilikiwa na Shetani. Ushindi wa Mungu dhidi ya Shetani ni mtindo usioepukika! Shetani kwa hakika alishindwa kitambo sana. Wakati injili ilipoanza kuenezwa kote duniani mwa joka kubwa jekundu, yaani, wakati Mungu mwenye mwili alipoanza kufanya kazi na kazi hii ikafanywa kuendelea, Shetani aliweza kushindwa kabisa, kwani kupata mwili wa Kristo kulimaanisha kumshinda Shetani. Shetani aliona kwamba Mungu alikuwa kwa mara nyingine tena amekuwa mwili na alikuwa ameanza kutekeleza kazi Yake, na akaona kwamba hakuna nguvu ambazo zingeweza kukomesha kazi hii. Hivyo basi, alipigwa na bumbuazi alipoona kazi hii na hakuthubutu kufanya kazi yoyote nyingine zaidi. Kwanza Shetani alifikiria kwamba pia alimiliki hekima nyingi, na akaingilia kati na kunyanyasa kazi ya Mungu; hata hivyo, hakutarajia kwamba Mungu alikuwa kwa mara nyingine tena amekuwa mwili, na kwamba katika kazi Yake, Mungu alikuwa ametumia uasi Wake kuhudumu kama ufunuo na hukumu kwa binadamu; na hivyo basi kumshinda binadamu na kumshinda Shetani. Mungu ni mwenye busara kumshinda, na kazi Yake

inamzidi Shetani kwa mbali. Hivyo basi, Niliwahi kutaja awali kwamba: Kazi Ninayoifanya inatekelezwa kutokana na ujanja wa Shetani. Mwishowe Nitafichua uweza Wangu na hali ya kutoweza kwa Shetani. Mungu anapofanya kazi Yake, Shetani anamfuata unyo unyo kutoka nyuma mpaka mwishowe anaangamizwa—hatajua hata kilichomgonga! Ataweza kutambua tu ukweli baada ya kuvunjwa na kupondwapondwa; na wakati huo atakuwa tayari amechomwa kwenye ziwa la moto. Hatakuwa ameshawishika kabisa wakati huo? Kwani hatakuwa na njama zozote zingine za kutumia!

Ni kazi hii ya kihalisi ya hatua kwa hatua ambayo mara nyingi inaulemea moyo wa Mungu kwa huzuni ya binadamu, kiasi kwamba vita Vyake na Shetani vimedumu kwa sasa miaka 6,000. Hivyo basi Mungu alisema hivi: “Sitawahi tena kuumba binadamu, wala kuwahi tena kuwapa malaika mamlaka.” Kuanzia hapo, wakati malaika walipokuja kufanya kazi duniani, walimfuata tu Mungu ili kufanya kazi fulani. Hakuwahi kuwapa malaika mamlaka. Je, malaika ambao Waisraeli waliwaona walitekeleza vipi kazi yao? Walijifichua katika ndoto na kupitisha maneno ya Yehova. Wakati Yesu alipofufuka siku tatu baada ya kusulubishwa, ni malaika ndio waliolisukuma jiwe kando; Roho wa Mungu hakufanya kazi hii yeye binafsi. Malaika waliweza kufanya tu kazi ya aina hii; walifanya tu wajibu wa usaidizi na hawakuwa na mamlaka, kwani Mungu hangewahi tena kuwapatia mamlaka. Baada ya kufanya kazi kwa muda fulani, watu ambao Mungu alitumia hapa duniani walichukua nafasi ya Mungu na kusema, “Nataka kuzidi ulimwengu! Nataka kusimama kwenye mbingu ya tatu! Tunataka hatamu za mamlaka ya ukuu!” Wangekuwa na kiburi baada ya siku kadhaa za kazi; walitaka mamlaka ya ukuu duniani, walitaka kuanzisha taifa jingine, walitaka vitu vyote viwe katika utawala wao na walitaka kusimama katika mbingu ya tatu. Je, kwani hujui kwamba wewe ni binadamu tu unayetumiwa na Mungu? Unawezaje kupaa hadi kwenye mbingu ya tatu? Mungu huja duniani kufanya kazi, kimyakimya na bila ya kujitangaza, na Huondoka baada ya kukamilisha kazi Yake kimyakimya. Hajitangazi kama vile binadamu wanavyofanya, lakini badala yake Anatekeleza kazi Yake kwa uhalisi. Wala haingii kanisani na kujitangaza, “Nitawaangamiza nyinyi nyote! Nitawalaani na kuwaadibu!” Anatekeleza tu kazi Yake binafsi, na kuondoka mara Anapomaliza. Wale wachungaji wa kidini wanaowaponya wagonjwa na kupunga mapepo, wanawasomea wengine kutoka kwenye madhabahu, na kutoa hotuba ndefu na zenye makuu na kuzungumzia masuala yasiyo ya kihalisi, wana kiburi hadi moyoni! Wao ni vizazi vya malaika mkuu!

Baada ya kufanya kazi Yake ya miaka 6,000 hadi leo, Mungu tayari amefichua vitendo Vyake vingi, sababu ya kimsingi ikiwa ni kumshinda Shetani na kuleta wokovu kwa binadamu wote. Anatomia fursa hii kuruhusu kila kitu mbinguni, kila kitu kilicho duniani, kila kitu kinachopatikana baharini pamoja na kila kifaa cha mwisho ambacho Mungu aliumba ulimwenguni kuweza kuona uweza wa Mungu na kushuhudia vitendo vyote vya Mungu. Yeye

huchukua fursa ya kumshinda Shetani ili kufichua vitendo Vyake kwa binadamu na kuwaruhusu watu kuweza kumsifu Yeye na kuitukuza hekima Yake kwa kumshinda Shetani. Kila kitu duniani, mbinguni na ndani ya bahari humletea utukufu, huusifu uweza Wake, kinasifu vitendo Vyake vyote na kutamka kwa sauti jina Lake takatifu. Hii ni ithibati ya ushindi Wake dhidi ya Shetani; hii ni ithibati ya Yeye kumshinda Shetani; na la muhimu zaidi, ni ithibati ya wokovu Wake kwa binadamu. Viumbe wote wa Mungu humletea utukufu, humsifu Yeye kwa kumshinda adui Wake na kurudi kwa ushindi na humsifu Yeye kama Mfalme mkubwa mwenye ushindi. Kusudio Lake si kumshinda Shetani tu, na hivyo basi kazi Yake imeendelea kwa miaka 6,000. Anatumia kushindwa kwa Shetani kuwaokoa binadamu; Anakutumia kushindwa kwa Shetani kufichua vitendo Vyake vyote na kufichua utukufu Wake wote. Atapata utukufu, na umati wote wa malaika utaweza kushuhudia utukufu Wake wote. Wajumbe walio mbinguni, wanadamu walio duniani na viumbe wote walio duniani watauona utukufu wa Muumba. Hii ndiyo kazi Aifanyayo. Viumbe vyake kule mbinguni na duniani vyote vitaona utukufu Wake, na Atarudi kwa vifijo na nderemo baada ya kumshinda Shetani kabisa na kumruhusu binadamu amsifu Yeye. Ataweza hivyo basi kutimiza kwa ufanisi vipengele hivi viwili. Mwishowe binadamu wote watashindwa na Yeye, na atamwondoa yeyote yule anayepinga au kuasi, hivi ni kusema, Atawaondoa wale wote wanaomilikiwa na Shetani. Unaviona vitendo hivi vyote vya Mungu sasa, ilhali ungali unapinga na unakuwa mwasi na hutaki kunyenyekea; unayahifadhi mambo mengi ndani yako na unafanya utakacho; unafuata ashiki zako, na kile upendacho—huu ni uasi; huu ni upingaji. Imani katika Mungu ambayo inatekelezwa kwa ajili ya mwili, kwa ajili ya ashiki za mtu, na kwa ajili ya kile anachopenda mtu, kwa ajili ya ulimwengu, na kwa ajili ya Shetani ni chafu; ni upinzani na uasi. Kunazo aina zote tofauti za imani sasa: Baadhi hutafuta hifadhi dhidi ya janga, na wengine hutafuta kupokea baraka, huku baadhi wakitamani kuelewa mafumbo na bado wengine hujaribu kupata pesa. Hiyo yote ni mifumo ya upinzani; hiyo yote ni kukufuru! Kusema kwamba mtu anapinga au anaasi—huku si kwa mujibu wa mambo haya? Watu wengi sasa hivi wanalalamika, wanatamka manung'uniko au kutoa hukumu. Haya yote ni mambo yanayofanywa na waovu; wao ni binadamu wapinzani na waasi; watu kama hao wamemilikiwa na kujawa na Shetani. Watu ambao Mungu huwapata ni wale wanaonyenyekea Kwake kabisa, wale waliopotoshwa na Shetani lakini wameokolewa na kushindwa na kazi Yake sasa, wale waliovumilia majaribu na hatimaye wamepokelewa kabisa na Mungu na hawaishi tena katika umiliki wa Shetani na wamevunja minyororo ya udhalimu, walio radhi kuishi kwa kudhihirisha utakatifu—hawa ndio watu watakatifu zaidi; hawa ndio wale watakatifu. Kama matendo yako ya sasa hayalingani na sehemu moja ya mahitaji ya Mungu utaondolewa. Hili halipingiki. Kila kitu kinafanywa kulingana na leo; ingawa Amekuamulia awali na kukuchagua wewe, matendo yako leo bado yataamua matokeo yako. Kama huwezi kuenda sambamba sasa, utaondolewa. Kama huwezi kuenda sambamba sasa, utawezaje kuenda sambamba baadaye? Sasa kwa kuwa muujiza

mkubwa kama huo umekufanyikia wewe, bado huamini. Basi, utamwamini vipi baadaye wakati Atakapomaliza kazi Yake na Hafanyi tena kazi kama hiyo? Wakati huo itakuwa vigumu zaidi kwako wewe kumfuata Yeye! Baadaye Mungu atategemea mwelekeo na maarifa yako katika kazi ya Mungu mwenye mwili na kile ulichopitia wewe ili kuamua kama wewe ni mwenye dhambi au mwenye haki, au kuamua kama wewe ndiwe uliyekamilishwa ama ni yule aliyeondolewa. Lazima uweze kuona wazi sasa. Roho Mtakatifu hufanya kazi hivyo: Yeye huamua matokeo yako kulingana na tabia yako leo. Nani anayeongea maneno ya leo? Nani anayefanya kazi ya leo? Nani anayeamua kama utaondolewa leo? Nani anayeamua kukufanya kuwa mtimilifu? Je, hiki sicho Ninachofanya Mimi mwenyewe? Mimi ndimi Ninayeongea maneno haya; Mimi ndimi Ninayeteteleza kazi hii. Kulaani, kuadibu na kuhukumu watu vyote ni sehemu ya kazi Yangu binafsi. Hatimaye, kukuondoa kutakuwa pia kazi Yangu binafsi. Yote ni shughuli Yangu binafsi! Kukufanya kuwa mtimilifu ni shughuli Yangu binafsi, na kukuruhusu kufurahia baraka ni shughuli Yangu binafsi pia. Hii yote ni shughuli Yangu binafsi. Matokeo yako hayakuamuliwa awali na Yehova; yanaamuliwa leo na Mungu wa leo. Yanaamuliwa sasa; hayakuamuliwa kabla ya ulimwengu kuumbwa. Baadhi ya watu wapumbavu husema, “Pengine kuna jambo mbaya na macho Yako, na Hunioni mimi kama vile Unavyofaa kuniona. Hatimaye mtaona namna Roho atakavyoonyesha kila kitu!” Yesu kwanza Alimchagua Yuda kama mwanafunzi Wake. Watu huuliza: “Angewezaje kumchagua mwanafunzi ambaye angemsaliti?” Mwanzo Yuda hakuwa na nia ya kumsaliti Yesu. Hili jambo lilifanyika tu baadaye. Wakati huo Yesu alikuwa amemchukua Yuda kwa upendo; Alimfanya mtu huyo amfuata Yeye na kumfanya awajibikie masuala yao ya kifedha. Kama Angejua kwamba Yuda angebadhiri pesa, Asingemwacha asimamie pesa hizo. Mtu anaweza kusema kwamba Yesu hakujua mwanzo kwamba mtu huyu hakuwa mwaminifu na alikuwa mdanganyifu, na kwamba aliwadanganya ndugu zake. Baadaye, baada ya Yuda kumfuata Yesu kwa muda fulani, Yesu alimwona Yuda akiwadanganya ndugu zake na kumrairai Mungu. Watu waligundua pia kwamba siku zote angetumia pesa kutoka kwenye mfuko wa fedha na kisha wakamwambia Yesu. Yesu alipata habari tu kuhusu haya yote wakati huu. Kwa sababu Yesu alikuwa ateteleze kazi ya kusulubishwa na Alihitaji mtu wa kumsaliti, na Yuda alitokea tu kuwa mhusika mzuri wa wajibu huu, Yesu akasema, “Kutakuwepo miongoni mwenu ambaye atanisaliti Mimi. Mwana wa Adamu atatumia usaliti huu kuweza kusulubishwa na baada ya siku tatu atafufuka.” Wakati huo Yesu hakuchagua hasa Yuda ili aweze kumsaliti Yeye; kinyume cha mambo ni kwamba, Alipenda kwamba Yuda awe mwanafunzi mtiifu. Bila kutarajia, Yuda aligeuka kuwa mlafi na aliyepotoka aliyemsaliti Bwana, na akatumia hali hii kumchagua Yuda kwa kazi hii. Kama wanafunzi wote kumi na wawili wa Yesu wangukuwa watiifu, na hakuna mtu kama Yuda angekuwa miongoni mwao, yule mtu wa kumsaliti Yesu angekuwa hatimaye mtu kutoka nje ya wale wanafunzi. Hata hivyo, wakati huo ilifanyika tu kwamba kulikuwa na mmoja miongoni

mwao aliyefurahia kuchukua hongo—Yuda. Yesu kwa hivyo basi alimtumia mtu huyu kukamilisha kazi Yake. Jambo hili lilikuwa rahisi jinsi gani! Yesu hakuliamua awali mwanzoni mwa kazi Yake; Alifanya tu uamuzi huu punde tu mambo yalipoimarika hadi hatua fulani. Huu ulikuwa ni uamuzi wa Yesu, yaani, uamuzi wa Roho wa Mungu Mwenyewe. Wakati huo ni Yesu aliyemchagua Yuda; wakati Yuda alipomsaliti Yesu baadaye, haya yalikuwa ni matendo ya Roho Mtakatifu ili kuhudumia hatima Zake mwenyewe; ilikuwa ni kazi ya Roho Mtakatifu wakati huo. Wakati Yesu alipomchagua Yuda, Hakuwa na wazo lolote kwamba Angemsaliti. Alijua tu kwamba alikuwa Yuda Iskariote. Matokeo yenu yanaamuliwa pia kulingana na kiwango chenu cha kunyenyekea leo na kulingana na kiwango chenu cha ukuaji wa maisha, na wala si kulingana na wazo miongoni mwa dhana za binadamu kwamba ilikuwa imepangiwa awali katika uumbaji wa ulimwengu. Lazima uelewe mambo haya waziwazi. Kazi hii nzima haitekelezwi kulingana na kufikiria kwako.

Kuhusu Majina na Utambulisho

Iwapo unataka kufaa kwa ajili ya matumizi na Mungu, lazima ujue kazi ya Mungu; lazima ujue kazi Aliyofanya awali (katika Agano Jipya na la Kale), na, zaidi ya hayo, lazima ujue kazi Yake ya leo. Ndiyo kusema, ni lazima uzitambue hatua tatu za kazi ya Mungu ya zaidi ya miaka 6,000. Ukiulizwa ueneze injili, basi hutaweza kufanya hivyo bila kuijua kazi ya Mungu. Mtu fulani anaweza kukuuliza kuhusu kile Mungu wenu amesema kuhusu Biblia, Agano la Kale, na kazi na maneno ya Yesu ya wakati huo. Ikiwa huwezi kunena kwa hadithi ya ndani ya Biblia, basi hawatashawishika. Mwanzoni, Yesu alizungumzia sana Agano la Kale na wanafunzi Wake. Kila kitu walichosoma kilitoka Agano la Kale; Agano Jipya liliandikwa tu miongo kadhaa baada ya kusulubiwa kwa Yesu. Kueneza injili, mnapaswa hasa kufahamu ukweli wa ndani wa Biblia, na kazi ya Mungu katika Israeli, ndiyo kusema kazi Aliyoifanya Yehova. Na pia mnapaswa kuelewa kazi aliyoifanya Yesu. Haya ndiyo sanasana maswala ambayo watu wote wana wasiwasi nayo, na hadithi ya ndani ya zile hatua mbili za kazi ndiyo hawajasikia. Wakati wa kueneza injili, kwanza weka kando majadiliano juu ya kazi ya Roho Mtakatifu leo. Hii hatua ya kazi hawawezi kufikia, kwa sababu mnachotafuta ni kile kilicho juu kuliko zote: maarifa ya Mungu, na maarifa ya kazi ya Roho Mtakatifu, na hakuna kilichopandishwa cheo zaidi ya hizi mbili. Ukizungumzia kwanza kilicho juu, itakuwa ni kubwa mno kwao, kwani hakuna ambaye amepitia kazi kama hiyo ya Roho Mtakatifu; haina historia, na si rahisi kwa mwanadamu kukubali. Uzoefu wao ni mambo ya kale kutoka zamani, pamoja na baadhi ya kazi ya Roho Mtakatifu. Wanayopitia si kazi ya leo ya Roho Mtakatifu, ama mapenzi ya Mungu leo. Bado wanatenda kulingana na mazoea ya kale, bila mwangaza mpya wala mambo mapya.

Katika enzi ya Yesu, Roho Mtakatifu hasa alifanya kazi Yake ndani ya Yesu, wakati wale

waliomtumikia Bwana wakivaa mavazi ya kuhani hekaluni walifanya hivyo kwa uaminifu uliodumu. Wao pia walikuwa na kazi ya Roho Mtakatifu, lakini hawakuweza kuhisi mapenzi ya sasa ya Mungu, na wakabakia tu waaminifu kwa Yehova kulingana na mazoea ya kale, bila uongozi mpya. Yesu alikuja na kuleta kazi mpya. Wale watu waliohudumu hekaluni hawakuwa na uongozi mpya wala hawakuwa na kazi mpya. Wakihudumu hekaluni wangeweza tu kutetea mazoea ya kale; bila kuondoka hekaluni, hawangeweza kuwa na kuingia kupya. Kazi mpya ililetwa na Yesu, na Yesu hakuvingia hekaluni kufanya kazi Yake. Alifanya kazi yake nje ya hekalu pekee, kwani wigo wa kazi ya Mungu ulikuwa umebadilika kitambo sana. Hakufanya kazi ndani ya hekalu, na mwanadamu alipomtumikia hapo ingeweza tu kuweka mambo yalivyokuwa, na haingeleta kazi yoyote mpya. Vivyo hivyo, watu wa dini bado huabudu Biblia leo. Ukieneza injili kwao, watakurushia maelezo ya juujuu ya maneno ya Biblia na watapata ushahidi mwingi, wakikuacha umezubaa na usijue la kusema; kisha watawawekea kipachiko and kuwaona kuwa wapumbavu katika imani yenu. Watasema, “Hujui hata Biblia, neno la Mungu, na unawezaje sema unamwamini Mungu?” Kisha watakudharau, na pia kusema, “Sababu mnayemwamini ni Mungu, mbona Asiweleze yote kuhusu Agano la Kale na Jipya? Sababu Ameleta utukufu Wake kutoka Israeli hadi upande wa Mashariki, mbona hajui kazi iliyoifanywa Israeli? Mbona hajui kazi ya Yesu? Kama hamjui, basi inathibitisha kwamba hamjalelezwa; sababu Yeye ndiye kupata mwili kwa Yesu kwa mara ya pili, ingewezekanaje kuwa hajui mambo haya? Yesu alijua kazi aliyoifanya Yehova; Angekosaje?” Wakati utakapofika, wote watakuuliza maswali kama haya. Vichwa vyao vimejaa mambo kama haya; watakosaje kuuliza? Wale walio katika mkondo huu hawazingatii Biblia, kwa vile mmetazama hatua kwa hatua kazi aliyoifanya Mungu leo, mmeshuhudia hii kazi ya hatua kwa hatua kwa macho yenu, mmeona wazi hatua tatu za kazi, na kwa hivyo imewabidi kuweka chini Biblia na kukoma kuitafiti. Lakini hawawezi kukosa kuitafiti, kwani hawana ujuzi wa hii kazi ya hatua kwa hatua. Watu wengine watauliza, “Nini tofauti kati ya kazi aliyoifanya Mungu wa mwili na ile ya manabii na mitume wa zamani? Daudi pia aliitwa Bwana, na hivyo pia akawa Yesu; ingawa kazi waliyoifanya ilikuwa tofauti, waliitwa kitu kimoja. Mbona, unauliza, hawakuwa na utambulisho mmoja? Kile Yohana alichoshuhudia kilikuwa maono, moja iliyotoka pia kwa Roho Mtakatifu, na aliweza kuyasema maneno ambayo Roho Mtakatifu alikusudia kuyasema; kwa nini utambulisho wa Yohana ni tofauti na ule wa Yesu?” Maneno aliyoyasema Yesu yaliweza kumwakilisha Mungu kikamilifu, na kuwakilisha kikamilifu kazi ya Mungu. Kile alichokiona Yohana kilikuwa maono, na hakuweza kuwakilisha kikamilifu kazi ya Mungu. Ni kwa nini Yohana, Petro na Paulo walizungumza maneno mengi—kama alivyofanya Yesu—lakini bado hawakuwa na utambulisho sawa na Yesu? Ni hasa kwa sababu kazi waliyoifanya ilikuwa tofauti. Yesu aliwakilisha Roho wa Mungu, na Alikuwa Roho wa Mungu Akifanya kazi moja kwa moja. Alifanya kazi ya enzi mpya, kazi ambayo hakuna aliyekuwa amefanya mbeleni. Yeye Alifungua njia mpya,

Alimwakilisha Yehova, na Alimwakilisha Mungu Mwenyewe. Ihali kwa Petro, Paulo na Daudi, bila kujali walichoitwa, waliwakilisha tu utambulisho wa kiumbe wa Mungu, na walitumwa na Yesu na Yehova. Kwa hivyo bila kujali kiasi cha kazi walichofanya, bila kujali jinsi walivyofanya miujiza kubwa, walikuwa bado tu viumbe wa Mungu, na hawakuweza kuwakilisha Roho Mtakatifu. Walifanya kazi kwa jina la Mungu ama baada ya kutumwa na Mungu; zaidi ya hayo, walifanya kazi katika enzi iliyoanzishwa na Yesu ama Yehova, na kazi waliyoifanya haikutengwa. Walikuwa, hatimaye, viumbe wa Mungu tu. Katika Agano la Kale, manabii wengi walizungumza utabiri, ama kuandika vitabu vya unabii. Hakuna aliyesema kuwa yeye ni Mungu, lakini punde tu Yesu Alipoanza kufanya kazi, Roho wa Mungu Alimshuhudia kuwa Yeye ni Mungu. Mbona hivyo? Kwa sasa, unapaswa kujua tayari! Awali, mitume na manabii waliandika nyaraka mbalimbali, na kufanya unabii mwingi. Baadaye, watu walichagua baadhi zao kuweka katika Biblia, na baadhi zikapotea. Kwa vile kuna watu wanaosema kuwa vitu vyote wanavyozungumza vimetoka kwa Roho Mtakatifu, mbona baadhi yavyo vinachukuliwa kuwa nzuri, na baadhi yavyo vinachukuliwa kuwa mbaya? Na mbona baadhi vilichaguliwa, na sio vingine? Kama kweli yalikuwa maneno Aliyoyasema Roho Mtakatifu, ingekuwa lazima kwa watu kuyachagua? Kwa nini akaunti ya maneno yaliyosemwa na Yesu na kazi Aliyoifanya ni tofauti katika kila moja ya Injili Nne? Makosa sio ya waliyoyarekodi? Watu wengine watauliza, “Sababu nyaraka zilizoandikwa na Paulo na waandishi wengine wa Agano Jipya na kazi walizozifanya zilitokana kidogo na matakwa ya mwanadamu, na zilichanganywa na dhana za mwanadamu, basi hakuna uchafu wa binadamu katika maneno ambayo Wewe (Mungu) unazungumza leo? Je, kweli hayana dhana hata moja za mwanadamu?” Hii hatua ya kazi aliyoifanya Mungu ni tofauti kabisa na zile walizozifanya Paulo na wengi wa mitume na manabii. Sio tu kwamba kuna tofauti na utambulisho, lakini, hasa, kuna tofauti kati ya kazi inayofanywa. Baada ya Paulo kupigwa chini na kuanguka mbele ya Bwana, aliongozwa na Roho Mtakatifu kufanya kazi, na akawa mtume. Na hivyo akaandikia makanisa nyaraka, na hizi nyaraka zote zilifuata mafundisho ya Yesu. Paulo alitumwa na Bwana kufanya kazi kwa jina la Bwana Yesu, lakini Mungu Mwenyewe alipokuja, Hakufanya kazi kwa jina lolote na Hakuwakilisha yeyote isipokuwa Roho wa Mungu katika kazi Yake. Mungu alikuja kufanya kazi Yake moja kwa moja: Hakukamilishwa na mwanadamu, na kazi Yake haikufanywa juu ya mafundisho ya mwanadamu yeyote. Katika hatua hii ya kazi Mungu haongozi kwa kuzungumza juu ya uzoefu Wake binafsi, ila Hufanya kazi Yake moja kwa moja, kulingana na Alichochacho. Kwa mfano, jaribio la watoa huduma, nyakati za kuadibu, jaribio la kifo, nyakati za kumpenda Mungu.... Hii yote ni kazi ambayo haijawahi kufanywa mbeleni, na ni kazi ya enzi ya sasa, badala ya uzoefu wa binadamu. Kwa maneno Nimesema, ni yapi mazoefu ya mwanadamu? Je, yote hayatoki moja kwa moja kwa Roho Mtakatifu, na hayatolewi nje na Roho Mtakatifu? Ni vile tu aina yako ni maskini sana hadi huwezi kuona kupitia ukweli! Maisha ya vitendo

Ninayozungumzia ni ya kuongoza njia, na hayajawahi zungumziwa na yeyote mbeleni, wala hakuna aliye na uzoefu wa njia hii, wala kujua ukweli huu. Kabla Niliyatamka maneno haya, hakuna aliyewahi kuyasema. Hakuna aliyezungumzia mazoefu haya, wala hakuna aliyewahi kusema maelezo hayo, na, zaidi ya hayo, hakuna aliyewahi kuonyesha hali kama hizo kufichua mambo haya. Hakuna aliyewahi kuongoza njia Ninayoongoza leo, na kama ingeongozwa na mwanadamu, basi isingekuwa njia mpya. Chukua Paulo na Petro, kwa mfano. Hawakuwa na uzoefu wao binafsi kabla ya Yesu aiongoze njia. Ilikuwa tu baada ya Yesu kuongoza njia ndipo walipopata uzoefu wa maneno aliyoyasema Yesu, na njia aliyoiongoza; kutoka hapa walipata mazoefu mengi, na kuziandika nyaraka, Na hivyo, uzoefu wa mwanadamu sio sawa na kazi Ya Mungu, na kazi ya Mungu sio sawa na maarifa yalivyoelezwa na dhana na uzoefu wa mwanadamu. Nimesema, tena na tena, kuwa leo Ninaongoza njia mpya, na kufanya kazi mpya, na kazi na matamshi Yangu ni tofauti na yale ya Yohana na wale manabii wengine wote. Kamwe, Sijawahi pata uzoefu kwanza, na kisha kuyazungumzia kwenu—hiyo sio ukweli hata kidogo. Kama ingekuwa hivyo, haingewachelewesha kitambo sana? Zamani, maarifa waliyoyazungumzia wengi yalipandishwa cheo pia, lakini maneno yao yote yalisemwa tu kulingana na hayo ya wanaoitwa takwimu wa kiroho. Hawakuiongoza njia, lakini walitoka kwa uzoefu wao, walitoka kwa walichokiona, na kwa maarifa yao. Zingine zilikuwa dhana zao, na mengine yalikuwa mazoefu waliyofupisha. Leo, asili ya kazi Yangu ni tofauti kabisa na yao. Sijapata uzoefu wa kuongozwa na wengine, wala Sijakubali kukamilishwa na wengine. Zaidi ya hayo, yote Nimesema na kushiriki ni tofauti na yale ya wengine, na hayajawahi kuzungumzwa na mwingine yeyote. Leo, bila kujali ninyi ni nani, kazi yenu inafanywa kulingana na maneno Nisemayo. Bila haya matamshi na kazi, nani angeweza kupata uzoefu wa mambo haya (majaribu ya watendaji huduma, nyakati za kuadibu...), na nani ataweza kuzungumzia maarifa kama haya? Kweli huna uwezo wa kuona haya? Bila kujali hatua ya kazi, punde tu maneno Yangu yasemwapo, mnaanza kushiriki kulingana na maneno Yangu, na kufanya kazi kulingana nayo, na sio njia ambayo yeyote kati yenu amefikiria. Baada ya kuja mbali hivi, huna uwezo wa kuona swali wazi na rahisi hivi? Sio njia iliyowazwa na yeyote, wala haijalinganishwa na mtu yeyote wa kiroho. Ni njia mpya, na hata maneno mengi yaliyosemwa mara kwanza na Yesu hayatumiki tena. Ninachozungumza ni kazi ya kufungua enzi mpya, na ni kazi inayosimama peke yake; kazi Nifanyayo, na maneno Nizungumzayo, yote ni mapya. Si hii ndiyo kazi mpya ya leo? Kazi ya Yesu pia ilikuwa hivi. Kazi Yake pia ilikuwa tofauti na hizo za watu wengine hekaluni, na pia ilitofautiana na kazi za Mafarisayo, na wala haikufanana na zilizofanywa na watu wote wa Israeli. Baada ya kuishuhudia, watu walishindwa kuamua: “Kweli ilifanywa na Mungu?” Yesu hakuzingatia sheria ya Yehova; Alipokuja kumfunza mwanadamu, yote Aliyoyanena yalikuwa mapya na tofauti na yale yaliyosemwa na watakatifu wa zamani na manabii wa Agano la Kale, na kwa sababu hii, watu walisalia bila uhakika. Hii ndiyo humfanya mwanadamu kuwa mgumu

sana kushughulika naye. Kabla ya kukubali hii hatua mpya ya kazi, njia ambayo wengi wenu walitembelea ilikuwa ya kutenda na kuingia katika msingi wa watu hao wa kiroho. Lakini leo, kazi Ninayoifanya ni tofauti sana, na hivyo hamna uwezo wa kuamua kama ni sawa ama sio. Sijalishwi na njia uliyopitia mbeleni, wala Sijali ulikula “chakula” cha nani, ama uliyemchukua kama “babako.” Sababu Nimekuja na kuleta kazi mpya ya kumwongoza mwanadamu, wote wanaonifuata lazima watende kulingana na Ninachosema. Bila kujali jinsi ulivyotoka “familia” ya nguvu, lazima unifuata, hupaswi kutenda kulingana na mazoea yako ya awali, “Baba wa kambo” wako anapaswa kushuka nawe unapaswa kuja mbele ya Mungu wako kupata mgao wako halali. Uzima wako wote umo mikononi Mwangu, nawe hupaswi kuwa na imani kipofu nyingi kwa baba wako wa kambo, hawezi kukutawala kabisa. Kazi ya leo inasimama peke yake. Yote Nisemayo leo ni wazi hayajalinganishwa na msingi wa zamani; ni mwanzo mpya, na ukisema kuwa umetengenezwa na mkono wa mwanadamu, basi wewe ni mtu aliye kipofu sana kwamba huwezi kuokolewa!

Isaya, Ezekieli, Musa, Daudi, Ibrahimu na Danieli walikuwa viongozi ama manabii kati ya wateule wa Israeli. Mbona hawakuitwa Mungu? Mbona Roho Mtakatifu hakuwashuhudia? Mbona Roho Mtakatifu alimshuhudia Yesu punde tu Alipoanza kazi yake na kuanza kuzungumza maneno Yake? Na mbona Roho Mtakatifu hakuwashuhudia wengine? Wao, wanadamu waliokuwa na mwili, wote waliitwa “Bwana.” Bila kujali waliyoiitwa, kazi yao inawakilisha utu wao na kiini chao, na utu wao na kiini chao kinawakilisha utambulisho wao. Kiini chao hakina uhusiano na majina yao, inawakilishwa na waliyoonyesha, na waliyoishi kwa kudhihirisha. Kwa Agano la Kale, hakuwa na chochote tofauti na kuitwa Bwana, na mtu angeitwa kwa njia yoyote, lakini kiini na utambulisho wake wa asili ulikuwa haubadiliki. Kati ya hao Kristo wa uwongo, manabii waongo na wadanganyifu, hakuna wanaoitwa “Mungu” pia? Na mbona hao sio Mungu? Kwa sababu hawana uwezo wa kufanya kazi ya Mungu. Mizizini, wao ni wanadamu, wanaowadanganya watu, sio Mungu, na hivyo hawana utambulisho wa Mungu. Daudi pia hakuitwa Bwana miongoni mwa makabila kumi na mawili? Yesu pia aliitwa Bwana: mbona ni Yesu pekee aliyeitwa Mungu wa mwili? Yereimia pia hakujulikana kama Mwana wa Adamu? Na Yesu pia hakujulikana kama Mwana wa Adamu? Mbona Yesu alisulubiwa kwa niaba ya Mungu? Si kwa sababu kiini chake kilikuwa tofauti? Si kwa sababu kazi aliyoifanya ilikuwa tofauti? Je, jina lina umuhimu? Ingawa Yesu pia aliitwa Mwana wa Adamu, Alikuwa kupata mwili kwa Mungu kwa mara ya kwanza. Alikuwa amekuja kuchukua mamlaka, na kukamilisha kazi ya ukombozi. Hii inathibitisha kuwa utambulisho na kiini cha Yesu kilikuwa tofauti na kile cha wengine waliyoiitwa pia wana wa wanadamu. Leo, nani kati yenu anathubutu kusema kwamba maneno yote yaliyotamkwa na wale waliotumiwa na Roho Mtakatifu yalitoka kwa Roho Mtakatifu? Kuna anayethubutu kusema mambo kama haya? Ukisema mambo kama

haya, basi mbona kitabu cha Ezra cha unabii kiliondolewa, na mbona jambo hilo pia likafanyiwa vitabu vya watakatifu na manabii wa kale? Kama yote yalitoka kwa Roho Mtakatifu, basi mbona mnathubutu kufanya maamuzi ambayo yanabadilika kama haya? Umehitimu kuchagua kazi ya Roho Mtakatifu? Hadithi nyingi kutoka Israeli pia zilitolewa. Na ukiamini kwamba maandishi haya yote ya kale yalitoka Roho Mtakatifu, basi mbona baadhi ya vitabu vilitolewa? Kama yote yalitoka kwa Roho Mtakatifu, yote yanapaswa kuwekwa, na kutumwa kwa ndugu na dada wa makanisa kuyasoma. Hayapaswi kuchaguliwa na kutolewa kwa matakwa ya mwanadamu; ni makosa kufanya hivyo. Kusema kwamba mazoe fu ya Paulo na Yohana yalichanganywa na waliyoyaona binafsi hakumaanishi kwamba uzoefu na maarifa yao yalitoka kwa Shetani, ila tu walikuwa na mambo yaliyotoka kwa mazoe fu na waliyoyaona wao binafsi. Maarifa yao yalilingana na asili ya mazoe fu halisi ya wakati huo, na ni nani anayeweza kusema kwa ujasiri kwamba yote yalitoka kwa Roho Mtakatifu? Kama Injili Nne zote zilitoka kwa Roho Mtakatifu, basi ilikuwaje kwamba Mathayo, Marko, Luka na Yohana kila mmoja alisema jambo tofauti kuhusu kazi ya Yesu? Msipoamini haya, basi angalia akaunti tofauti kwa Biblia ya jinsi Petro alivyomkana Yesu mara tatu: Yote ni tofauti, na kila moja ina sifa yake yenyewe. Wengi walio wajinga husema, “Mungu wa mwili pia ni mwanadamu, kwa hivyo maneno Anayoyazungumza yanaweza kutoka kikamilifu kwa Roho Mtakatifu? Kama maneno ya Paulo na Yohana yalichanganywa na matakwa ya mwanadamu, basi maneno Anayoyasema kweli hayajachanganywa na matakwa ya mwanadamu?” Watu wanaosema mambo kama haya ni vipofu na wajinga! Soma Injili Nne kwa kina; soma iliyorekodi kuhusu alichofanya Yesu, na maneno Aliyoyasema. Kila akaunti ilikuwa kwa urahisi tofauti, na kila ilikuwa na mtazamo wake. Kama vilivyoandikwa na waandishi wa vitabu hivi vyote vilitoka kwa Roho Mtakatifu, basi yote yanapaswa kuwa sawa na thabiti. Basi mbona kuna tofauti? Si mwanadamu ni mjinga sana, kutoweza kuona haya? Ukiulizwa kutoa ushuhuda kwa Mungu, ni ushuhuda upi unaoweza kutoa? Njia hii ya kumjua Mungu inaweza kumshuhudia? Wengine wakikuuliza, “Kama rekodi ya Yohana na Luka yalichanganywa na matakwa ya mwanadamu, basi maneno yanayosemwa na Mungu wenu hayajachanganywa na matakwa ya mwanadamu?” utaweza kupeana jibu wazi? Baada ya Luka na Mathayo kuyasikia maneno ya Yesu, na kuona kazi ya Yesu, walizungumzia maarifa yao, kwa namna ya kumbukumbu walisema kwa kina baadhi ya mambo aliyoyafanya Yesu. Unaweza kusema kwamba maarifa yao yalifichuliwa kabisa na Roho Mtakatifu? Nje ya Biblia, kulikuwa na watu wengi wa kiroho wa maarifa ya juu kuwaliko; mbona maneno yao hayajachukuliwa na vizazi vya baadaye? Wao hawakutumika pia na Roho Mtakatifu? Jua kwamba kwa kazi ya leo, Sizungumzii juu ya kuona kwangu kunaolingana na msingi wa kazi ya Yesu, wala Sizungumzi juu ya maarifa Yangu dhidi ya usuli wa kazi ya Yesu. Ni kazi ipi Aliyofanya Yesu wakati huo? Na ni kazi ipi Ninayofanya leo? Ninachofanya na kusema hayana historia. Njia Nitembeleayo leo haijawahi kukanyagiwa mbeleni, haikuwahi tembelewa na watu

wa enzi na vizazi vya kale. Leo, imefunguliwa, na hii sio kazi ya Roho? Hata kama ilikuwa kazi ya Roho Mtakatifu, viongozi wote wa kale walifanya kazi yao juu ya msingi wa wengine. Hata hivyo, kazi ya Mungu Mwenyewe ni tofauti. Hatua ya kazi ya Yesu ilikuwa sawa: Aliifungua njia mpya. Alipokuja Alihubiri injili ya ufalme wa mbinguni, na kusema kwamba mwanadamu anapaswa kutubu na kukiri. Baada ya Yesu kukamilisha kazi yake, Petro na Paulo na wengineo walianza kuendeleza kazi ya Yesu. Baada ya Yesu kusulubiwa na kupaa mbinguni, walitumwa na Roho Mtakatifu kueneza njia ya msalaba. Ingawa maneno ya Paulo yalipandishwa cheo, pia yalilingana na msingi uliolazwa na kile Yesu alisema, kama uvumilivu, upendo, mateso, kufunika kichwa, ubatizo, ama mafundisho mengine yakufuatwa. Haya yote yalikuwa juu ya msingi wa maneno ya Yesu. Hawakuwa na uwezo wa kufungua njia mpya, kwani wote walikuwa wanadamu waliotumiwa na Mungu.

Matamshi na kazi ya Yesu wakati huo hayakushikilia mafundisho, na hakufanya kazi Yake kulingana na kazi ya sheria ya Agano la Kale. Yalilingana na kazi iliyopaswa kufanywa kwa Enzi ya Neema. Alitenda kulingana na kazi Aliyokuwa amelea mbele, kulingana na mipango Yake, na kulingana na huduma Yake; Hakufanya kazi kulingana na sheria ya Agano la Kale. Hakuna Alichofanya kilicholingana na Agano la Kale, na Hakuja kufanya kazi ili kutimiza maneno ya manabii. Kila hatua ya kazi ya Mungu haikuwa wazi ili kutimiza utabiri wa manabii wa zamani, na Hakuja kuyafuata mafundisho au kutambua makusudi utabiri wa manabii wa kale. Bado vitendo Vyake havikuvuruga utabiri wa manabii wa kale, wala havikuvuruga kazi Aliyokuwa amefanya awali. Hatua muhimu ya kazi Yake haikuwa kufuata mafundisho yoyote, na kufanya kazi ambayo Yeye Mwenyewe anapaswa kufanya. Yeye hakuwa nabii wala mwaguzi, ila mtendaji, aliyekuja kufanya hiyo kazi Aliyopaswa kufanya, na aliyekuja kufungua enzi Yake mpya na kufanya kazi Yake mpya. Bila shaka, Yesu alipokuja kufanya kazi Yake, pia Alitimiza maneno mengi yaliyosemwa na manabii wa zamani kwa Agano la Kale. Hivyo pia kazi ya leo imetimiza utabiri wa manabii wa zamani wa Agano la Kale. Ni vile tu Sishikili hiyo “kalenda njano ya zamani,” hayo tu. Kwani kuna kazi zaidi ambayo lazima Nifanye, kuna maneno zaidi ambayo lazima Niwazungumzie, na kazi hii na maneno haya ni ya umuhimu mkubwa kuliko kueleza vifungu kutoka Biblia, kwa sababu kazi kama hiyo haina maana ama thamani kubwa kwenu, na haiwezi kuwasaidia, au kuwabadilisha. Ninanuia kufanya kazi mpya sio kwa ajili ya kutimiza kifungu chochote kutoka Biblia. Ikiwa Mungu alikuja duniani tu kutimiza maneno ya manabii wa Biblia, basi ni nani aliye mkuu, Mungu wa mwili ama hao manabii wa zamani. Na hata hivyo, hao manabii ni wasimamizi wa Mungu, ama Mungu ni msimamizi wa manabii? Unaweza kueleza haya maneno jinsi gani?

Mwanzoni, wakati Yesu alikuwa bado hajafanya rasmi huduma Yake, kama wanafunzi waliomfuata, wakati mwingine pia Yeye alihudhuria mikutano, na kuimba tenzi, Akasifu, na

kusoma Agano la Kale kwa hekalu. Baada Yeye kubatizwa na kupanda, Roho alishuka rasmi juu yake na kuanza kufanya kazi, Akifichua utambulisho Wake na huduma Aliyokuwa afanye. Kabla ya haya, hakuna aliyejua utambulisho Wake, na mbali na Maria, hata Yohana hakujuu. Yesu alikuwa 29 Alipobatizwa. Baada ya ubatizo wake kukamilika, mbingu zilifunguliwa, na sauti ikasema: “Huyu ni Mwana wangu Mpendwa, ambaye Ninapendezwa naye.” Baada ya Yesu kubatizwa, Roho Mtakatifu alianza kumshuhudia kwa njia hii. Kabla ya kubatizwa Akiwa na umri wa 29, Alikuwa ameishi maisha ya ukawaida wa mtu, kula wakati Alipotakiwa kula, kulala na kuvaa kawaida, na hakuna chochote kumhusu kilikuwa tofauti. Bila shaka hii ilikuwa tu kwa nyama ya macho ya mwanadamu. Wakati mwingine Alikuwa mnyonge sana, na wakati mwingine Hakuweza kupambanua mambo, kama tu ilivyoandikwa kwa Biblia Akili Yake ilikua pamoja na umri Wake. Haya maneno yanaonyesha tu kwamba Alikuwa na ubinadamu na kwamba Hakuwa hasa na tofauti na watu wengine ambao ni wa kawaida. Alikuwa pia amelelewa kama mtu wa kawaida, na hakuwa na chochote maalum kumhusu. Hata hivyo Alikuwa chini ya utunzaji na ulinzi wa Mungu. Baada ya kubatizwa, Alianza kujaribiwa, baada yake Akaanza kufanya Huduma Yake na kufanya kazi, na Alimiliki nguvu, hekima, na mamlaka. Hii si kusema kwamba Roho Mtakatifu hakufanya kazi ndani Yake kabla ya ubatizo Wake, ama hakuwa ndani Yake. Kabla ya ubatizo Wake Roho Mtakatifu pia aliishi ndani Yake lakini Hakuwa ameanza rasmi kazi Yake, kwani kuna mipaka ya wakati Mungu afanyapo kazi Yake, na zaidi ya hayo, watu wa kawaida wana mwendo kawaida wa kukua. Roho Mtakatifu alikuwa daima anaishi ndani Yake, Yesu alipozaliwa, Alikuwa tofauti na wengine, na nyota ya asubuhi ilionekana; kabla Yeye kuzaliwa, malaika alimtokea Yusufu kwa ndoto na kumweleza kuwa Maria angejifungua mtoto wa kiume, na kwamba mtoto huyo alipatwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Baada ya Yesu kubatizwa, Roho Mtakatifu Alianza kazi Yake, lakini hili halimaanishi kwamba Roho Mtakatifu alikuwa tu amemshukia Yesu wakati huo. Huo msemu kwamba Roho Mtakatifu alishuka kama njiwa juu yake inamaanisha kuanza rasmi kwa huduma Yake. Roho wa Mungu alikuwa ndani yake mbeleni, lakini Hakuwa ameanza kufanya kazi, kwani wakati hukuwa umefika, na Roho hakuanza kazi upesi. Roho alimshuhudia kupitia ubatizo. Alipotoka nje ya maji, Roho alianza rasmi kufanya kazi ndani Yake, iliyoashiria kuwa Mungu wa mwili alikuwa ameanza kutimiza huduma Yake, na alikuwa ameanza kazi ya ukombozi, hiyo ni, Enzi ya Neema ilikuwa imeanza rasmi. Na hivyo, kuna wakati wa kazi Ya Mungu, bila kujali kazi Anayoifanya. Baada ya ubatizo Wake, hakukuwa na mabadiliko fulani kwa Yesu; Alikuwa bado ndani ya mwili wake kawaida. Ni kwamba tu alianza kazi Yake na kufichua utambulisho wake, na Alijawa na mamlaka na nguvu. Kwa swala hili, Alikuwa tofauti kuliko awali. Utambulisho wake ulikuwa tofauti, kusema kwamba kulikuwa na mabadiliko muhimu kwa hadhi Yake; huu ulikuwa ushahidi wa Roho Mtakatifu, na haikuwa kazi iliyofanywa na mwanadamu. Mwanzoni, watu hawakujua, na walikuja kujua kidogo wakati Roho Mtakatifu alimshuhudia Yesu kwa njia

hiyo. Kama Yesu angekuwa amefanya kazi kubwa kabla ya Roho Mtakatifu kumshuhudia, lakini bila shuhuda ya Mungu Mwenyewe, basi bila kujali jinsi kazi Yake ilivyokuwa kubwa, watu hawangejua kuhusu utambulisho Wake, kwani jicho la mwanadamu halingekuwa na uwezo wa kuiona. Bila hatua ya ushuhuda wa Roho Mtakatifu, hakuna ambaye angemtambua kama Mungu wa mwili. Kama, baada ya Roho Mtakatifu kumshuhudia, Yesu angeendelea kufanya kazi kwa njia hiyo hiyo, bila tofauti yoyote, basi haingekuwa na athari hiyo, na hii hasa imeonyeshwa kwa kazi ya Roho Mtakatifu pia. Baada ya Roho Mtakatifu kuwa na ushuhuda, Roho Mtakatifu alipaswa kujionyesha Mwenyewe, ili uweze kuona wazi kuwa Alikuwa Mungu, kwamba kulikuwa na Roho wa Mungu ndani Yake; ushuhuda wa Mungu hukukosea, na hii ingethibitisha kwamba ushuhuda Wake ulikuwa sahihi. Iwapo kazi ya kabla na baada ya ushuhuda wa Roho Mtakatifu ingekuwa sawa, basi huduma Yake ya mwili na kazi ya Roho Mtakatifu hazingekuwa maarufu, na hivyo mwanadamu hangekuwa na uwezo wa kutambua kazi ya Roho Mtakatifu, kwani hakuwa na tofauti wazi. Baada ya kuwa na ushuhuda, Roho Mtakatifu alilazimika kutetea huu ushuhuda, na hivyo ilimlazimu kuonyesha hekima na mamlaka Yake ndani ya Yesu, ambayo ilikuwa tofauti na wakati wa kale. Bila shaka, hii haikuwa athari ya ubatizo; ubatizo ni sherehe tu, ni kwamba tu ubatizo ulikuwa njia ya kuonyesha kwamba ulikuwa wakati wa kufanya huduma Yake. Kazi hiyo ilikuwa ya kufanya wazi nguvu kubwa za Mungu, kufanya wazi ushuhuda wa Roho Mtakatifu, na Roho Mtakatifu angechukua jukumu la ushuhuda huu mpaka mwisho. Kabla ya kufanya huduma Yake, Yesu pia alisikiliza mahubiri, Alihubiri na kueneza injili katika maeneo mbalimbali. Hakufanya kazi yoyote kubwa kwa sababu muda bado hukuwa umewadia ili Afanye huduma Yake, na pia kwa sababu Mungu Mwenyewe alijificha kwa unyenyekevu ndani ya mwili, na Hakufanya kazi yoyote hadi wakati ulipofika. Hakufanya kazi kabla ya ubatizo kwa sababu mbili: Kwanza, kwa sababu Roho Mtakatifu hakuwa ameshuka rasmi juu Yake kufanya kazi (ndiyo kusema, Roho Mtakatifu hakuwa amempea Yesu nguvu na mamlaka ya kufanya kazi kama hii), na hata kama Angekuwa anajua utambulisho Wake Mwenyewe, Yesu hangeweza kufanya kazi Aliyonuia kufanya baadaye, na ingembidi kusubiri hadi siku Yake ya ubatizo. Huu ulikuwa wakati wa Mungu, na hakuna ambaye angeweza kuikiuka, hata Yesu Mwenyewe; Yesu Mwenyewe hangeweza kuipinga kazi Yake Mwenyewe. Bila shaka, huu ulikuwa unyenyekevu wa Mungu, na pia sheria ya kazi ya Mungu; Kama Roho wa Mungu hangefanya kazi, hakuna ambaye angeweza kufanya kazi Yake. Pili, kabla Yeye kubatizwa, Alikuwa tu mwanadamu wa kawaida sana, bila tofauti na watu wa kawaida; hiki ni kipengele kimoja cha jinsi Mungu wa mwili alikuwa kawaida. Mungu wa mwili hakuenda kinyume na mipango ya Roho wa Mungu; Alifanya kazi kwa njia taratibu na kawaida. Ilikuwa tu baada ya kubatizwa ndipo kazi Yake ilikuwa na nguvu na mamlaka. Ambayo ni kusema, hata kama alikuwa Mungu wa mwili, Hakufanya matendo yasiyo ya kawaida, na Alikua kwa njia sawa na watu wa kawaida. Kama Yesu alikuwa ashaujua utambulisho wake, Alikuwa amefanya

kazi kubwa eneo yote kabla ya ubatizo Wake, na Alikuwa tofauti na watu wa kawaida, kujionyesha Mwenyewe kuwa ajabu, basi haingewezekana tu kwa Yohana kufanya kazi yake, lakini pia hakungekuwa na njia ya Mungu kuanza hatua ifuatayo ya kazi Yake. Na hivyo hii ingethibitisha kwamba alichofanya Mungu kilienda mrama, na kwa mwanadamu, ingeonekana kuwa Roho wa Mungu na Mungu wa mwili hawakutoka mahali moja. Hivyo, kazi ya Yesu iliyorekodiwa kwa Biblia ni kazi iliyofanywa baada ya Yeye kubatizwa, kazi iliyofanywa katika kipindi cha miaka mitatu. Biblia haijarekodi Alichofanya kabla ya kubatizwa kwa sababu Hakufanya kazi hii kabla ya kubatizwa. Alikuwa tu mtu wa kawaida, na Aliwakilisha mtu wa kawaida; kabla ya Yesu kuanza kufanya huduma Yake, Hakuwa na tofauti na watu wa wenye ukawaida, na wengine hawangeona tofauti yoyote na yeye. Ilikuwa tu baada ya Yeye kufikia 29 ndipo Yesu alijua kwamba Alikuwa amekuja kukamilisha hatua ya kazi ya Mungu; kabla; Yeye Mwenyewe hakujua, kwani kazi Aliyofanya Mungu ilikuwa kawaida. Alipohudhuria mkutano kwa sinagogi Akiwa na umri wa miaka kumi na miwili, Maria alikuwa akimtafuta, na alisema tu sentensi moja kwa namna sawa na mtoto mwingine yeyote: “Mama! Hujui kwamba ni lazima Niyaweke mapenzi ya Baba Yangu juu ya mengine yote?” Bila shaka, kwa vile alitwawa mwili na tendo la Roho Mtakatifu, Yesu hangeweza kuwa maalum kwa namna fulani? Lakini umaalum Wake hukumaanisha hakuwa kawaida, ila tu kuwa Alimpenda Mungu zaidi ya mtoto mwingine mdogo. Ingawa Alionekana kama mwanadamu, kiini Chake bado kilikuwa maalum na tofauti na cha wengine. Lakini, ilikuwa tu baada ya ubatizo ndipo Alipohisi Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani Yake, ndipo Alipohisi kuwa Mungu Mwenyewe. Ni baada tu na Yeye kuhitimu miaka 33 ndipo Alitambua kweli kuwa Roho Mtakatifu alinuia kufanya kazi ya usulubisho kupitia kwake. Akiwa na umri wa miaka 32, Alikuwa kujua baadhi ya ukweli wa ndani, kama tu ilivyoandikwa kwa Injili ya Mathayo: “Naye Simoni Petro akajibu na kusema, Wewe ndiye Kristo, Mwana wa Mungu aishiye. ... Kutoka wakati huo kuendelea Yesu alianza kuwaonyesha wanafunzi Wake, jinsi ilivyompasa kwenda Yerusalemu, na kupitia mateso mengi ya wazee na makuhani wakuu na waandishi, na kufishwa, na afufuke tena siku ya tatu.” Hakujua awali kazi Aliyotakiwa kufanya, lakini kwa wakati maalum. Hakujua kwa kina punde tu Alipozaliwa; Roho Mtakatifu alifanya kazi polepole ndani Yake, na kulikuwa na mchakato wa kazi. Kama, hapo mwanzoni, Angejua kuwa yeye ni Mungu, na Kristo, na Mwana wa Adamu wa mwili, kwamba Alikuwa akamilishe kazi ya usulubisho, basi mbona Hakufanya kazi awali? Mbona tu baada ya kuwaeleza wanafunzi Wake kuhusu huduma Yake ndipo Yesu alipohisi huzuni, na kusali kwa bidii kwa ajili ya hii? Mbona Yohana alimfungulia njia na kumbatiza kabla ya Yeye kuelewa mambo mengi ambayo Hakuyaelewa? Kinachothibitishwa na hii ni kwamba ilikuwa kazi ya Mungu wa mwili, na hivyo ili aelee, na kutimiza, kulikuwa na mwendo, kwani alikuwa Mungu wa mwili, na kazi Yake ilikuwa tofauti na ile iliyofanywa moja kwa moja na Roho.

Kila hatua ya kazi ya Mungu hufuata mkondo mmoja na sawa, na hivyo katika mpango wa usimamizi wa Mungu wa miaka elfu sita, kila hatua imefuatwa kwa karibu na ifuatayo, kutoka msingi wa dunia hadi leo. Kama hakungekuwa na mtu wa kupisha njia, hakungekuwa na mtu wa kuja baadaye; Kwani kuna wale wanaokuja baadaye, kuna wale wanaopisha njia. Kwa njia hii kazi imepitishwa chini, hatua kwa hatua. Hatua moja inafuata ingine, na bila mtu wa kufungua njia, haitawezekana kuanza kazi, na Mungu angekosa namna ya kupeleka kazi Yake mbele. Hakuna hatua inayopingana na nyingine, na kila hatua inafuata nyingine katika mlolongo kuunda mkondo; hii yote inafanywa na Roho Yule Yule. Lakini bila kujali iwapo mtu atafungua njia ama kuendeleza kazi ya mwingine, hii haiamui utambulisho wake. Hii si sawa? Yohana aliifungua njia, na Yesu akaendeleza kazi yake, hivyo hii inathibitisha kwamba utambulisho wa Yesu ni chini kuliko wa Yohana? Yehova alifanya kazi Yake kabla Yesu, hivyo unaweza kusema kuwa Yehova ni mkubwa kumliko Yesu? Iwapo waliopasha njia ama kuendeleza kazi za wengine sio muhimu; kilicho muhimu ni kiini cha kazi zao, na utambulisho unaowakilishwa. Hii si sawa? Kwa vile Yesu alinuia kufanya kazi miongoni mwa wanadamu, ilimbidi Awainue wale ambao wangepanya kazi ya kupasha njia. Yohana alipoanza tu kuhubiri, alisema, “Itayarisheni ninyi njia ya Bwana, yafanyeni mapito Yake kuwa nyooofu.” “Ninyi tubuni: kwa kuwa ufalme wa mbinguni uko karibu.” Aliongea hivi tangu mwanzoni, na mbona aliweza kuyasema maneno haya? Kwa suala la utaratibu ambao maneno haya yalisemwa, ni Yohana aliyezungumzia kwanza injili ya ufalme wa mbinguni, na Yesu aliyezungumza baadaye. Kulingana na dhana za mwanadamu, ni Yohana aliyeifungua njia mpya, na bila shaka Yohana alikuwa mkubwa kumliko Yesu. Lakini Yohana hakusema yeye ni Kristo, na Mungu hakumshuhudia kama Mwana mpendwa wa Mungu, lakini Alimtumia tu kufungua na kuandaa njia ya Bwana. Alimpisha Yesu njia, lakini hangefanya kazi kwa niaba ya Yesu. Kazi zote za mwanadamu pia zilidumishwa na Roho Mtakatifu.

Katika enzi ya Agano la Kale, ni Yehova aliyeongoza njia, na kazi ya Yehova iliwakilisha enzi nzima ya Agano la Kale, na kazi zote zilizofanywa Israeli. Musa tu alizingatia hizi kazi duniani, na kazi zake zinachukuliwa kuwa ushirikiano uliotolewa na mwanadamu. Wakati huo, Yehova ndiye aliyezungumza, na Akimwita Musa, na Alimwinua Musa miongoni mwa watu wa Israeli, na kumfanya awaongoze nyikani na kuendelea hadi Kanaani. Hii haikuwa kazi ya Musa mwenyewe, lakini hiyo iliyoagizwa kibinafsi na Yehova, na hivyo Musa hawezi kuitwa Mungu. Musa pia aliweka chini sheria, lakini sheria hii iliamrisha kibinafsi na Yehova. Ni kwamba tu alifanya Musa kuitaja. Yesu pia alitengeneza amri, na kuondoa sheria ya Agano la Kale na kuweka amri ya enzi jipya. Mbona Yesu ni Mungu Mwenyewe? Kwa sababu haya si mambo sawa. Wakati huo, kazi aliyoifanya Musa haikuwakilisha enzi, wala haikufungua njia mpya; alielekezwa mbele na Yehova, na alikuwa tu anatumiwa na Mungu, Yesu alipokuja, Yohana

alikuwa amefanya hatua ya kazi ya kupisha njia, na alikuwa ashaanza kueneza injili ya ufalme wa mbinguni (Roho Mtakatifu alikuwa ameanza hii). Yesu alipokuja, Alifanya moja kwa moja kazi Yake Mwenyewe, lakini kulikuwa na tofauti kubwa kati ya kazi Yake na kazi ya Musa. Isaya pia alizungumzia unabii mwingi, lakini mbona yeye hakuwa Mungu Mwenyewe? Yesu hakuzungumzia unabii mwingi lakini mbona Alikuwa Mungu Mwenyewe? Hakuna aliyethubutu kusema kwamba kazi zote za Yesu wakati huo zilitoka kwa Roho Mtakatifu, wala hawathubutu kusema zote zilitoka kwa matakwa ya mwanadamu, ama kwamba zilikuwa kabisa kazi za Mungu Mwenyewe. Mwanadamu hakuwa na njia yoyote ya kuchambua mambo haya. Inaweza kusemwa kwamba Isaya alifanya kazi kama hiyo, na kuzungumzia unabii huo, na yote yalitoka kwa Roho Mtakatifu; hayakutoka moja kwa moja kwa Isaya mwenyewe, lakini yalikuwa ufunuo kutoka kwa Yehova. Yesu hakufanya kazi nyingi sana, na Hakusema maneno mengi sana, wala Hakuzungumzia unabii mwingi. Kwa mwanadamu, mahubiri Yake hayakuonekana hasa ya kupandishwa cheo, lakini alikuwa Mungu Mwenyewe, na mwanadamu hawezi kueleza haya. Hakuna aliyewahi kumwamini Yohana, ama Isaya, ama Daudi, wala hakuna aliyewahi kuwaita Mungu, ama Daudi Mungu ama Yohana Mungu, hakuna aliyewahi kuzungumza hivi, na ni Yesu tu aliyewahi kuitwa Kristo. Uainishaji huu umefanywa kulingana na ushahidi wa Mungu, kazi Aliyoifanya, na huduma Aliyoifanya. Kuhusu watu wakuu wa Biblia—Ibrahimu, Daudi, Yoshua, Danieli, Isaya, Yohana na Yesu—kupitia kazi waliyoifanya, unaweza kusema ni nani aliyekuwa Mungu Mwenyewe, na ni watu wapi walio manabii, na ni wapi walio mitume. Ni nani aliyetumiwa na Mungu, na nani aliyekuwa Mungu Mwenyewe, inatofautishwa na kuamuliwa na asili na aina za kazi walizozifanya. Iwapo huwezi kusema tofauti, basi hii inadhihirisha kwamba hujui maana ya kumwamini Mungu. Yesu ni Mungu kwa sababu Alizungumza maneno mengi, na kufanya kazi nyingi hasa maonyesho Yake ya miujiza nyingi. Vivyo hivyo, Yohana, pia alifanya kazi nyingi, na kuzungumza maneno mengi, Musa pia; mbona hawakuitwa Mungu? Adamu aliumbwa moja kwa moja na Mungu; mbona hakuitwa Mungu, badala tu ya kuitwa kiumbe? Mtu akikwambia, “Leo, Mungu amefanya kazi nyingi sana, na kuzungumza maneno mengi; Yeye ni Mungu Mwenyewe. Basi, vile Musa alivyozungumza maneno mengi, lazima yeye pia ni Mungu Mwenyewe!” inapaswa uwarudishie swali, “Wakati huo, mbona Mungu alimshuhudia Yesu, na sio Yohana, kama Mungu Mwenyewe? Je, Yohana hakumtangulia Yesu? Ni ipi iliyokuwa kubwa, kazi ya Yohana ama Yesu? Kwa mwanadamu, kazi ya Yohana inakaa mkubwa kuliko ya Yesu, lakini mbona Roho Mtakatifu alimshuhudia Yesu, na sio Yohana?” Hiki kitu kimoja kinafanyika leo! Mwanzoni, Musa alipowaongoza watu wa Israeli, Yehova alimwongelesha kutoka miongoni mwa mawingu. Musa hakuzungumza moja kwa moja lakini badala yake aliongozwa moja kwa moja na Yehova. Hii ilikuwa kazi ya Israeli ya Agano la Kale. Ndani ya Musa hamkuwa na Roho, ama nafsi ya Mungu. Hangeweza kufanya kazi hiyo, na hivyo kuna tofauti kubwa kati ya aliyoifanya na Yesu. Na hiyo ni kwa sababu kazi walizozifanya

zilikuwa tofauti! Iwapo mtu anatumiwa na Mungu, ama ni nabii, mtume, ama Mungu Mwenyewe, unaweza kubainishwa na asili ya kazi yake, na hii itakomesha mashaka yenu, Kwa Biblia, imeandikwa kwamba Kondoo peke yake ndiye anayeweza kuivunja mihuri saba. Kupitia zama zote kumekuwa na wachambuzi wengi wa maandiko miongoni mwa watu wakuu, na hivyo unaweza kusema kwamba wote ni Kondoo? Unaweza kusema kwamba maelezo yao yote yalitoka kwa Mungu? Walikuwa tu wachambuzi; hawana utambulisho wa Kondoo. Wanastahilije kuivunja mihuri saba? Ni ukweli kwamba “Kondoo peke yake anaweza kuivunja mihuri saba,” Lakini Hakuji tu kuivunja mihuri saba; hakuna umuhimu wa kazi hii, inafanywa kwa bahati. Yeye yu wazi kabisa kuhusu kazi Yake Mwenyewe; ni muhimu Kwake kutumia muda mwingi kutafsiri maandiko? Ni lazima “Enzi ya Mwanakondoo Akitafsiri Maandiko” iongezwe kwa kazi ya miaka elfu sita? Anakuja kufanya kazi mpya, lakini pia Anatoa ufunuo kadhaa kuhusu kazi za nyakati za zamani, kufanya watu waelewe ukweli wa kazi ya miaka elfu sita. Hakuna haja ya kueleza vifungo vingi kutoka Biblia; kazi ya leo ndiyo iliyo kuu, hiyo ni muhimu. Unapaswa kujua kwamba Mungu haji hasa kuivunja mihuri saba, ila kufanya kazi ya wokovu.

Unajua tu kuwa Yesu atashuka siku za mwisho, lakini atashuka jinsi gani hasa? Mwenye dhambi kama wewe, aliyetoka tu kukombolewa, na hajabadilishwa bado, ama kukamilishwa na Mungu, unaweza kuufuata roho wa Mungu? Kwa wewe, wewe ambaye ni wa nafsi yako ya zamani, ni kweli kuwa uliokolewa na Yesu, na kwamba huhesabiwi kama mwenye dhambi kwa sababu ya wokovu wa Mungu, lakini hii haithibitishi kwamba wewe si mwenye dhambi, na si mchafu. Unawezaje kuwa mtakatifu kama haujabadilishwa? Ndani, umezingirwa na uchafu, ubinafsi na ukatili, na bado unatamani kushuka na Yesu—huwezi kuwa na bahati namna hiyo! Umepitwa na hatua moja katika imani yako kwa Mungu: umekombolewa tu, lakini haujabadilishwa. Ili uipendeze nafsi ya Mungu, lazima Mungu Mwenyewe afanye kazi ya kukubadilisha na kukutakasa; ikiwa umekombolewa tu, hautakuwa na uwezo wa kufikia utakatifu. Kwa njia hii hautahitimu kushiriki katika baraka nzuri za Mungu, kwani umepitwa na hatua kwa kazi ya Mungu ya kusimamia mwanadamu, ambayo ni hatua muhimu ya kubadilisha na kukamilisha. Na basi wewe, mwenye dhambi aliyetoka tu kukombolewa, huna uwezo wa kurithi urithi wa Mungu moja kwa moja.

Bila mwanzo wa hatua hii mpya ya kazi, ni nani ajuaye umbali upi ninyi wainjilisti, wahubiri, wachambuzi na wanaoitwa wanadamu wa kiroho wangeenda! Bila mwanzo wa hatua hii mpya ya kazi, mnachozungumzia ni cha zamani! Ama inapaa kwa kiti cha enzi, au kutayarisha kimo cha kuwa mfalme; ama kukanusha binafsi au kuhini mwili wa mtu; ama kuwa mtulivu au kujifunza masomo kutoka mambo yote; ama unyenyekevu au upendo. Hii ni kuimba wimbo sawa na zamani? Ni jambo tu ya kuita kitu kimoja na jina lingine! Ama kufunika kichwa

cha mtu na kuvunja mkate, au kuweka mikono na kuomba, na kuponya wagonjwa na kutoa mapepo. Kunaweza kuwa na kazi ingine mpya? Kunaweza kuwa na matarajio ya maendeleo? Ukiendelea kwa njia hii, utayafuata mafundisho kwa upofu, ama ufuate mkataba. Mnaamini kazi yenu kuwa ya juu mno, lakini hamjui kwamba yote yalipitiwa na kufundishwa na hao “watu wazee” wa nyakati za zamani? Yote mnayoyasema na kufanya si maneno ya mwisho ya hao watu wazee? Siyo malipo ya hawa watu wazee kabla wafariki? Unafikiri kuwa vitendo vyenu vinashinda vile vya mitume na manabii wa vizazi vilivyopita, na pia kushinda mambo yote? Mwanzo wa hatua hii ya kazi umetamatisha kuabudu kwenu kwa kazi ya Mshahidi Lee ya kutaka kuwa mfalme, na kupaa kwa kiti cha enzi, na kukamata kiburi na fujo yenu, kwa hivyo hamna uwezo wa kuingilia hatua hii ya kazi. Bila hatua hii ya kazi, mngezama hata zaidi katika kutokombolewa. Kuna mengi yaliyo mzee miongoni mwenu! Kwa bahati nzuri, kazi ya leo imewarudisha; kama si hivyo, nani anajua mwelekeo ambao mngechukua! Kwa kuwa Mungu ni Mungu ambaye daima ni mpya na kamwe si mzee, mbona hutafuti mambo mapya? Mbona daima unakwamilia mambo ya kale? Na hivyo, kuijua kazi ya Roho Mtakatifu leo una umuhimu mkubwa!

Wale Waliokamilishwa Pekee Ndio Wanaoweza Kuishi Maisha Yenye Maana

Kwa kweli, kazi inayofanywa sasa ni kuwafanya watu kumtoroka Shetani, kutoroka babu zao wa kale. Hukumu zote kwa neno zinalenga kufichua tabia potovu ya binadamu na kuwawezesha watu kuelewa kiini cha maisha. Hukumu hizi zote zilizorudiwa zinapenyeza mioyo ya watu. Kila hukumu inaathiri kwa njia ya moja kwa moja hatima yao na inalenga kujeruhi mioyo yao ili waweze kuachilia yale mambo hayo yote na hivyo basi kuja kujua maisha, kuujua ulimwengu huu mchafu, na pia kujua hekima ya Mungu na uweza Wake na kujua mwanadamu huyu aliyepotoshwa na Shetani. Kadri aina hii ya kuadibu na kuhukumu inavyozidi, ndivyo moyo wa binadamu unavyoweza kujeruhiwa zaidi na ndivyo roho yake inavyoweza kuzinduliwa zaidi. Kuzindua roho za watu hawa waliopotoka pakubwa na kudanganywa kabisa ndiyo shabaha ya aina hii ya hukumu. Mwanadamu hana roho, yaani, roho yake ilikufa kitambo na hajui kwamba kuna Mbingu, hajui kwamba kuna Mungu, na bila shaka hajui kwamba yeye mwenyewe anang’ang’ana kwenye lindi kuu la kifo; anaweza kujua kwamba anaishi katika kuzimu hii yenye maovu hapa ulimwenguni? Angewezaje kujua kwamba maiti hii yake ambayo imeoza, kwa kupotoshwa na shetani, imeanguka Kuzimuni kwenye kifo? Angewezaje kujua kwamba kila kitu hapa ulimwenguni kimeharibiwa kitambo kiasi cha kutokarabatika na mwanadamu? Na angewezaje kujua kwamba Muumba amekuja ulimwenguni leo na anatafuta kundi la watu waliopotoka ambao Anaweza kuokoa? Hata baada ya mwanadamu kupitia kila

usafishaji na hukumu inayowezezekana, ufahamu wake wa chini unashtuka kwa shida na kwa kweli hautikii chochote. Binadamu wamezoroteka kweli! Ingawa aina hii ya hukumu ni kama mvua katili ya mawe inyesayo kutoka mbinguni, ni yenye manufaa makubwa zaidi kwa binadamu. Kama isingekuwa ya kuhukumu watu hivi, kusingekuwa na matokeo yoyote na haingewezezekana kabisa kuwaokoa watu dhidi ya janga la umaskini. Kama isingekuwa kwa kazi hii, ingekuwa vigumu sana kwa watu kutoka Kuzimuni kwa sababu mioyo yao imekufa kitambo na roho zao kukanyagiwa kitambo na Shetani. Kuwaokoa nyinyi ambao mmeanguka kwenye kina kirefu cha uozo kunahitaji kuwaita kwa bidii sana, kuwahukumu kwa bidii sana, na kwa kufanya hivi tu ndipo mioyo hiyo yenu migumu itakapozinduka.

Miili yenu, matamania yenu ya kupita kiasi, ulafi wenu, na ashiki yenu vyote vimekita mizizi ndani yenu. Mambo haya yanaidhibiti sana mioyo yenu kiasi kwamba hamna nguvu za kutupa huo utumwa wa mawazo hayo ya kikabaila na yaliyooza. Hamtamani kubadilisha hali yenu ya sasa, wala kuukimbia ushawishi wa giza. Mmefanywa kuwa watumwa tu wa mambo hayo. Hata kama mnajua kwamba maisha kama hayo ni yenye maumivu sana na kwamba ulimwengu kama huo ni wenye giza la kupindukia, bado, hakuna hata mmoja wenu anao ujasiri wa kubadilisha maisha ya aina hii. Mnatamani tu kutoroka aina hii ya maisha halisi, kuondoa nafsi zenu kutoka kwenye mahali pa mateso ya muda na kuishi katika mazingira yenye amani, furaha na yafananayo na mbinguni. Hamko radhi kuvumilia magumu ili kuweza kubadilisha maisha yenu ya sasa; vilevile hamko radhi kutafuta ndani ya hukumu hii na kuadibu huku maisha ambayo mnafaa kuyaishi. Badala yake, mnaziota ndoto zisizo na uhalisi kabisa kuhusu ulimwengu mzuri wa nje ya miili yenu. Maisha mnayotamani ni yale mnayoweza kupata kwa urahisi bila kupitia maumivu yoyote. Hayo si ya kihalisi kamwe! Kwa sababu kile mnachotumainia si kuishi kwa kudhihirisha maisha ya maana katika mwili na kupata ukweli kwenye harakati ya maisha yenu, yaani, kuishi kwa ajili ya ukweli na kutetea haki. Haya siyo yale maisha ambayo mngedhani ni ya kupendeza, ya kuisimua. Mnahisi kwamba haya hayatakuwa maisha yanayovutia au ya maana. Machoni mwenu, kuishi maisha kama hayo kutatoa hisia za kudhalilishwa! Hata Ingawa mnakubali kuadibu huku leo, hata hivyo kile mnachofuatilia si kupata ule ukweli au kuishi kwa njia ya ukweli katika wakati wa sasa, bali kuweza kuingia katika maisha yenye furaha nje ya miili yenu baadaye. Hamtafuti ukweli wala hamtetei ukweli, wala hamtetei ukweli na bila shaka hampo kwa ajili ya kweli. Hamtafuti kuingia leo, lakini badala yake kila wakati mnafikiria “siku moja,” huku mkitazama mbingu ya samawati na kudondokwa na machozi machungu, na mkitarajia kuchukuliwa kuenda mbinguni siku moja. Je, hamjui kwamba kufikiria huku kama kwenu tayari kumeondokwa na uhalisi? Unaendelea kufikiria kwamba Mwokozi mwenye upole na huruma isiyoisha bila shaka atakuja siku moja kukuchukua pamoja na Yeye, wewe ambaye umevumilia ugumu na mateso

ulimwenguni humu, na kwamba Yeye bila shaka atalipiza kisasi kwa ajili yako wewe ambaye umedhalilishwa na kunyanyaswa. Je, si kweli kwamba umejaa dhambi? Wewe pekee ndiwe ambaye umeteseka ulimwenguni humu? Umilikiwa na Shetani wewe mwenyewe na kuteseka—je, bado Mungu anahitaji kukulipizia kisasi? Wale wasioweza kutosheleza mahitaji ya Mungu—kwani wao wote si adui wa Mungu? Wale wasioamini katika Mungu mwenye mwili—kwani wao si wapinga Kristo? Matendo yako mazuri yana maana gani? Yanaweza kuchukua nafasi ya moyo unaomwabudu Mungu? Huwezi kupokea baraka za Mungu kwa kufanya baadhi ya matendo mazuri tu, naye Mungu hatakulipizia kisasi yale mabaya uliyofanyiwa kwa sababu tu umeonewa na kukandamizwa. Wale wanaomwamini Mungu ilhali hawamjui Mungu, lakini wanaofanya matendo mazuri—kwani wao nao hawaadibiwi pia? Unamwamini Mungu tu, unataka Mungu akushughulikia na Akulipizie kisasi tu kwa mabaya uliofanyiwa wewe, na unataka Mungu kukupa njia ya kimbilio kutoka kwa umaskini wako. Lakini unataka kutilia maanani ukweli; wala hutamani kuishi kwa kudhihirisha ukweli. Hata zaidi, huwezi kuyakimbia maisha haya magumu na yasiyo na maana. Badala yake, huku ukiishi maisha yako katika mwili na maisha yako ya dhambi, unamwangalia Mungu kwa matarajio ya kusahihisha manung'uniko yako na kuondoa ukungu wa kuwepo kwako. Haya yanawezekanaje? Ukimiliki ukweli, unaweza kumfuata Mungu. Kama unaishi kwa kudhihirisha, unaweza kuwa onyesho la neno la Mungu. Kama unao uzima, unaweza kufurahia baraka ya Mungu. Ni wale tu walio na ukweli wanaweza kufurahia baraka ya Mungu. Mungu huhakikisha kwamba anawafidia wale wote wanaompenda kwa moyo wao wote pamoja na pia wanaovumilia magumu na mateso, na wala si kwa wale wanaojipenda tu na wamejipata kwenye mtego wa uwongo wa Shetani. Kunawezaje kuwa na wema miongoni mwa wale wasiopenda ukweli? Kunawezaje kuwa na haki miongoni mwa wale wanaopenda mwili tu? Si kweli kwamba haki na wema vyote vinarejelea ukweli? Si kweli kwamba vyote hivi vimehifadhiwa wale wanaompenda Mungu kwa moyo wao wote? Wale wasiopenda ukweli na ambao ni maiti zinazooza—je, watu hawa wote huwa hawajaficha maovu? Wale wasioweza kuishi ukweli—hawa wote si adui wa ukweli? Na je ninyi?

Kama unaweza kutoroka ushawishi huu wa giza na kujitenga na mambo hayo machafu, kama unaweza kuwa mtakatifu, inamaanisha kwamba unao ukweli. Si kwamba asili yako yamebadilika, lakini tu kwamba unaweza kuweka ukweli katika matendo na unaweza kuunyima mwili wako. Haya ndiyo yanayopatikana kwa wale waliotakaswa. Shabaha kuu ya kazi ya kushinda ni kuwatakaswa binadamu ili mwanadamu aweze kuwa na ukweli, kwa sababu mwanadamu sasa anauelewa ukweli kidogo sana! Kufanya kazi ya kushinda kwa watu hawa ni jambo la umuhimu mkubwa mno. Nyote mmeanguka katika ushawishi wa giza na mmeumizwa mno. Shabaha ya kazi hii, basi, ni kuwawezesha kujua asili ya binadamu na hivyo basi kuishi kwa ukweli. Kukamilishwa ni kitu ambacho viumbe wote wanafaa kukubali. Kama kazi ya

awamu hii inahusu tu kufanya watu kuwa wakamilifu, basi inaweza kufanywa Uingereza, au Amerika, au Israeli; inaweza kufanywa kwa watu wa taifa lolote. Lakini kazi ya kushinda ni kuwa inachagua. Hatua ya kwanza ya kazi ya kushinda ni ya muda mfupi; aidha, itatumika kumdhalilisha Shetani na kuushinda ulimwengu mzima. Hii ndiyo kazi ya mwanzo ya kushinda. Mtu anaweza kusema kwamba kiumbe yeyote anayemwamini Mungu anaweza kufanywa kuwa kamili kwa sababu kukamilishwa ni kitu ambacho mtu anaweza kufikia tu baada ya mabadiliko ya muda mrefu. Lakini kushindwa ni tofauti. Kielelezo na mlengwa wa kushinda lazima awe yule anayebaki nyuma zaidi, akiishi kwenye giza totoro kabisa, na vilevile mwenye hadhi kidogo kabisa, na asiyekuwa radhi kumkubali Mungu zaidi, na asiyetii Mungu zaidi. Huyu ndiye aina ya mtu anayeweza kutoa ushuhuda wa kushindwa. Shabaha kuu ya kazi ya kushinda ni kumshinda Shetani. Shabaha kuu ya kufanya watu kuwa wakamilifu, kwa upande mwingine, ni kuwapata watu wale. Ni kwa ajili ya kuwawezesha watu kuwa na ushuhuda baada ya kushindwa ndio kazi ya kushinda imewekwa hapa, kwa watu kama ninyi. Lengo ni kuwafanya watu kutoa ushuhuda baada ya kushindwa. Watu hawa walioshindwa watatumika kufikia shabaha ya kumdhalilisha Shetani. Kwa hivyo, mbinu kuu ya ushindi ni gani? Kuadibu, hukumu, kutupilia mbali laana, na kufichua—kutumia tabia ya haki katika kuwashinda watu ili waweze kushawishika kabisa kwa sababu ya tabia ya haki ya Mungu. Ili kutumia uhalisi wa neno na kutumia mamlaka ya neno ili kuwashinda watu na kuwashawishi kabisa—hii ndiyo maana ya kushindwa. Wale waliofanywa kuwa wakamilifu hawawezi tu kuwa watiifu baada ya kushindwa, lakini wanaweza pia kuwa na maarifa ya kazi ya hukumu, kubadilisha tabia yao na kumjua Mungu. Wanapitia njia ya kumpenda Mungu na wamejazwa na ukweli. Wanajua namna ya kupitia kazi ya Mungu, wanaweza kuteseka kwa ajili ya Mungu, na wanayo hiari zao wenyewe. Wale waliokamilishwa ni wale walio na ufahamu halisi wa ukweli kutokana na kupitia neno la Mungu. Wale walioshindwa ni wale wanaojua kuhusu ukweli lakini hawajakubali maana halisi ya ukweli. Baada ya kushindwa, wanatii, lakini utiifu wao wote unatokana na hukumu waliyopokea. Hawana uelewa kabisa wa hali halisi ya ukweli mwingi. Wanautambua ukweli kwa matamshi, lakini bado hawajapitia ukweli; wanauelewa ukweli, lakini hawajapitia ule ukweli. Kazi inayofanywa kwa wale wanaokamilishwa inajumuisha kuadibiwa na kuhukumiwa, pamoja na kupokea uzima. Mtu anayethamini kuingia katika ukweli ni mtu anayefaa kukamilishwa. Tofauti kati ya wale watakaofanywa kuwa wakamilifu na wale walioshindwa ni iwapo wanaingia ukweli. Wale wanauelewa ukweli, wameingia katika ukweli, na wanauishi ukweli huo ndio wale waliokamilishwa; wale wasioelewa ukweli, hawauingii ukweli, yaani, wale wasioishi ukweli, ni watu wasioweza kukamilishwa. Ikiwa watu kama hao wanaweza sasa kutii kabisa, basi wameshindwa. Kama wale walioshindwa hawatafuti ukweli—kama wanafuata lakini hawaishi kwa njia ya ukweli, kama wanaona na kuusikia ukweli lakini hawathamini kuthamini kuishi kwa njia ya ukweli—basi hawawezi kukamilishwa. Watu ambao ni wa kufanywa kuwa

wakamilifu wanatenda ukweli kulingana na mahitaji ya Mungu kwao katika njia ya ya kuelekea kukamilishwa. Kupitia haya, wanatimiza mapenzi ya Mungu, na wanapata kufanywa kuwa wakamilifu. Yeyote anayefuata hadi mwisho kabla ya kazi hiyo ya ushindi kuhitimishwa ni aliyeshindwa, lakini hawezi kusemekana kuwa ndiye aliyekamilishwa. Waliokamilishwa kunarejelea wale ambao, baada ya kumalizika kwa kazi ya ushindi, wanaweza kufuatilia ukweli na kumilikiwa na Mungu. Kunaashiria wale ambao, baada ya kukamilika kwa kazi ya ushindi, wanasimama imara katika majaribio na wanaishi kwa kudhihirisha ukweli. Kile kinachotofautisha kushindwa na kukamilishwa ni zile tofauti katika hatua za kufanya kazi na tofauti katika kiwango ambacho watu huelewa na kuingia katika ukweli. Wale wote ambao hawajaingia katika njia ya kukamilishwa, kumaanisha wale wasio na ukweli, mwishowe bado wataondolewa. Ni wale tu walio na ukweli na wanaoishi ukweli wanaoweza kumilikiwa kabisa na Mungu. Yaani, wale wanaoishi kwa kudhihirisha mfano wa Petro ndio wanaofanywa kuwa wakamilifu, huku wengine wote ndio ambao wameshindwa. Kazi inayofanywa kwa wale wote wanaoshindwa inajumuisha tu kuweka laana, kuadibu, na kuonyesha hasira, na yale yanayowajia ni haki na laana tu. Kushughulikia mtu kama huyo ni kufichua waziwazi—kufichua tabia potovu iliyo ndani yake ili aweze kuitambua mwenyewe na kushawishika kabisa. Punde binadamu anapokuwa mtiifu kabisa, kazi ya ushindi inakamilika. Hata kama watu wengi wangali hawatafuti kuelewa ukweli, kazi ya ushindi itakuwa imekamilika.

Kunacho kigezo cha kufikiwa iwapo utakamilishwa. Kupitia kwa uamuzi wako, ustahimilivu wako, na dhamiri yako, na kupitia ufuatiliaji wako, utaweza kupitia maisha na kutimiza mapenzi ya Mungu. Haya ndiyo kuingia kwako na kile kinachohitajika kwenye njia ya kuwa mkamilifu. Kazi ya kuwa mkamilifu inaweza kufanywa kwa watu wote. Yeyote anayemfuatilia Mungu anaweza kufanywa kuwa mkamilifu na anayo fursa na sifa za kufanywa kuwa mkamilifu. Hakuna sheria ngumu na ya haraka hapa. Ikiwa mtu anaweza kukamilishwa hasa kunategemea kile anachofuatilia. Watu wanaopenda ukweli na walio na uwezo wa kuishi kwa kudhihirisha ukweli bila shaka wanaweza kufanywa kuwa wakamilifu. Watu wasioupenda ukweli hawasifiwi na Mungu; hawamiliki maisha ambayo Mungu anadai, na hawawezi kufanywa kuwa kamilifu. Kazi ya kufanywa kuwa mkamilifu ni kwa minajili tu ya kuwamiliki watu, na wala si hatua katika kupigana na Shetani; kazi ya ushindi ipo tu kwa minajili ya kupigana na Shetani, kumaanisha kwamba kutumia ushindi wa mwanadamu ili kumzidi Shetani nguvu. Sehemu hii ya nyuma ndiyo kazi kuu, kazi mpya zaidi ambayo haijawahi kufanywa katika enzi zote. Mtu anaweza kusema kwamba shabaha ya hatua hii ya kazi kimsingi ni kuwashinda watu wote ili kuweza kumshinda Shetani. Kazi ya kufanya watu kuwa wakamilifu—hiyo si kazi mpya. Kazi yote katika kipindi ambapo Mungu anafanya kazi katika mwili inayo shabaha yake kuu kama ushindi wa watu. Hii ni sawa na ile Enzi ya Neema. Ukombozi wa

wanadamu wote kupitia kwa kusulubishwa ndiyo iliyokuwa kazi kuu. “Kuwapata watu” kulikuwa nyongeza katika kazi ya mwili na kulifanywa tu baada ya kusulubishwa. Wakati Yesu alipokuja na kufanya kazi Yake, shabaha Yake ilikuwa hasa kutumia kusulubishwa Kwake kushinda utumwa wa kifo na Kuzimu, kuweza kushinda ushawishi wa Shetani, kumaanisha kumshinda Shetani. Ilikuwa tu baada ya kusulubishwa kwa Yesu ndipo Petro alipoanza hatua kwa hatua kushika njia ya kuwa ukamilifu. Bila shaka alikuwa miongoni mwa wale waliomfuata Yesu wakati Yesu alipokuwa akifanya kazi, lakini hakufanywa kuwa mkamilifu wakati huo. Badala yake, ilikuwa ni baada ya Yesu kumaliza kazi Yake ndipo Petro alipoanza kuelewa taratibu ukweli na kisha akafanywa kuwa mkamilifu. Mungu mwenye mwili huja ulimwenguni tu kukamilisha hatua muhimu na ya maana sana ya kazi katika kipindi kifupi cha muda, si kuishi kwa kipindi kirefu miongoni mwa watu ulimwenguni na kuwafanya kuwa kamili kwa makusudi. Huwa hafanyi kazi hiyo. Hasubirii mpaka wakati ule ambao binadamu amefanywa kuwa mkamilifu kabisa ili kuhitimisha kazi Yake. Hiyo siyo shabaha na umuhimu wa kupata mwili Kwake. Yeye huja tu ili kufanya kazi ya kipindi kifupi ya kuwaokoa binadamu, na wala si kufanya ile kazi ya kipindi kirefu sana ya kuwafanya binadamu kuwa wakamilifu. Kazi ya kuwaokoa binadamu ni ya uwakilishi, inayoweza kuzindua enzi mpya na inaweza kukamilishwa katika kipindi kifupi cha muda. Lakini kuwafanya binadamu kuwa wakamilifu kunahitaji kuwaleta binadamu hadi kiwango fulani na ni kazi inayoweza kuchukua muda mrefu. Kazi hii lazima ifanywe na Roho wa Mungu, lakini inafanywa kwa msingi wa ukweli unaozungumzwa wakati wa kazi Yake akiwa mwili. Au aidha Yeye huwainua mitume kufanya kazi ya uchungaji ya kipindi kirefu, ili kufikia shabaha Yake ya kuwafanya binadamu kuwa wakamilifu. Mungu mwenye mwili hafanyi kazi hii. Huongea tu kuhusu njia ya maisha ili watu waweze kuelewa na kuwapatia tu binadamu ukweli, badala ya kuandamana na mwanadamu bila kusita katika kutenda ukweli kwani kufanya hivyo hakumo ndani ya huduma Yake. Kwa hivyo Hatakuwa akiandamana na mwanadamu mpaka siku ile ambayo mwanadamu ataelewa kabisa ukweli na kupata kabisa ukweli. Kazi Yake akiwa mwili inahitimishwa wakati mwanadamu anapoingia rasmi kwenye njia sahihi ya kumwamini Mungu, wakati mwanadamu anapoingia kwenye njia sahihi ya kufanywa kuwa mkamilifu. Hapa, bila shaka ndipo pia wakati ambapo atakuwa Ameshinda Shetani kabisa na kuutawala ulimwengu. Hajali kama mwanadamu hatimaye ameingia ukweli wakati huo, wala kujali kuhusu kama maisha ya binadamu ni makubwa au madogo. Hakuna kati ya hayo ambayo Yeye akiwa katika mwili anafaa kusimamia; hakuna kati ya hayo iko ndani ya huduma ya Mungu mwenye mwili. Punde Anapomaliza kazi aliyonua, Yeye huhitimisha kazi Yake katika mwili. Kwa hiyo, kazi ambayo Mungu mwenye mwili anafanya ni kazi ile tu ambayo Roho wa Bwana hawezi kufanya moja kwa moja. Aidha, ni ile kazi ya wokovu ya kipindi kifupi, na wala si kazi ya kipindi kirefu hapa ulimwenguni.

Kuinua ubora wa tabia zenu hakumo ndani ya eneo la kazi Yangu. Ninawaomba kufanya hivi tu kwa sababu ubora wa tabia yako uko chini sana. Kwa ukweli hii si sehemu ya kazi ya kukamilisha; badala yake, ni kazi ya ziada mnayofanyiwa ninyi. Kazi inayokamilishwa kwenu leo inafanywa kulingana na kile mnachohitaji. Imebinafsishwa, na wala si njia fulani inayofaa kuingiwa na kila mtu ambaye anafanywa kuwa mkamilifu. Kwa sababu ubora wenu wa tabia uko chini zaidi kuliko yeyote yule aliyefanywa kuwa mkamilifu kitambo, kazi hii, inapokuja kwenu, inakabiliwa na vizuizi vingi. Nimo miongoni mwenu nikifanya kazi hii ya ziada kwa sababu malengo ya kukamilisha ni tofauti. Kimsingi, wakati Mungu anapokuja ulimwenguni, Yeye hubaki ndani ya eneo Lake la kufaa na kutekeleza kazi Yake, bila kujishughulisha sana na shughuli nyingine. Hahusiki katika masuala ya familia au kushiriki katika maisha ya watu. Hajali kabisa kuhusu mambo hayo madogomadogo; yote haya si sehemu ya huduma Yake. Lakini ubora wako wa tabia uko chini zaidi kuliko vile Nilivyohitaji—hakuna ulinganifu kamwe—kiasi cha kwamba unakuwa kizuizi katika kazi. Aidha, kazi hii lazima ifanywe miongoni mwa watu katika nchi hii ambayo ni Uchina. Hamjapata elimu sana kiasi cha kwamba Sina chaguo lolote ila kuamuru kwamba muweze kupata elimu. Nimewaambieni kwamba hii ni kazi ya ziada, lakini pia ni kitu ambacho lazima muwe nacho, kitu kinachowafaidi nyinyi katika kufanywa kuwa mkamilifu. Kwa hakika, mnafaa kupata elimu, maarifa ya kimsingi kuhusu mienendo yenu binafsi, na maarifa ya kimsingi kuhusu maisha yaliyo mbele yenu; Sifai kuwazungumzia kuhusu mambo haya. Lakini kwa sababu hamna mambo haya, Sina chaguo jingine ila kufanya kazi ya kutia vitu hivi ndani yenu baada ya kuzaliwa humu ulimwenguni. Hata kama mna dhana nyingi kunihusu, bado Ninahitaji hiki kutoka kwenu, bado nahitaji kwamba muinue ubora wenu wa tabia. Si nia Yangu kuja na kufanya kazi hii, kwa sababu kazi Yangu ni kuwashinda tu, kupata imani yenu kamili kwa kuwahukumu nyinyi tu, hivyo basi kuonyesha njia ya maisha mnayofaa kuingia. Nikisema kwa njia nyingine, vile ambavyo mmeelimika na kama mna maarifa kuhusu maisha visingenihusu Mimi kamwe kama isingekuwa kwamba Nahitaji kuwashinda kwa neno Langu. Vyote hivi vinaongezewa ili kuhakikisha kuna matokeo yanayopatikana kutoka kwa kazi ya ushindi na kwa minajili ya kufanywa kwenu kuwa wakamilifu kutakakofuata. Si hatua ya kazi ya ushindi. Kwa sababu ubora wenu wa tabia ni wa hali ya chini, na nyie ni wavivu, na wazembe, wajinga, na wapumbavu, na wagumu na washenzi—kwa sababu nyie mmekithiri mipaka ya kutokuwa wenye akili razini—Nahitaji kwanza muinue ubora wenu wa tabia. Yeyote anayetaka kufanywa mkamilifu lazima afikie vigezo fulani. Ili kufanywa kuwa mkamilifu, lazima mtu awe wa akili razini na yenye umakinifu na awe radhi kuishi maisha yenye maana. Kama wewe ni mtu usiye radhi kuishi maisha matupu, mtu anayefuatilia ukweli, mtu aliye mwenye bidii katika kila kitu anachofanya, na mtu aliye na ubinadamu wa kawaida kabisa, basi wewe una sifa zinazostahili kufanywa kuwa mkamilifu.

Kazi hii miongoni mwenu inatekelezwa kwenu kulingana na ile kazi inayohitajika kufanywa. Baada ya ushindi wa watu hawa, kundi la watu litafanywa kuwa kamilifu. Kwa hivyo, kazi nyingi ya sasa pia inatayarisha shabaha ya kuwafanya kuwa wakamilifu, kwa sababu wapo wengi sana walio na hamu ya ukweli ambao wanaweza kufanywa kuwa wakamilifu. Kama kazi ya kushinda ilifaa kutekelezwa kwenu na baadaye kusiwe kazi ya ziada kufanywa, basi ni kwamba baadhi ya wale wanaotamani ukweli hawangepata? Kazi ya sasa inalenga kufungua njia ya kuwafanya watu kuwa wakamilifu baadaye. Ingawa kazi Yangu ni ya ushindi tu, njia ya maisha iliyotamkwa na Mimi hata hivyo ni inatayarisha kuwafanya watu kuwa wakamilifu baadaye. Kazi inayokuja baada ya ushindi inaweka msingi wa kukamilisha hukukamili, na hivyo basi ushindi unafanywa ili kuweka msingi wa kule kufanywa kuwa wakamilifu. Mwanadamu anaweza kufanywa kuwa mkamilifu baada ya kushindwa tu. Sasa hivi kazi kuu ni kushinda; baadaye wale wanaotafuta na kutamani ukweli watafanywa kuwa wakamilifu. Kufanywa kuwa mkamilifu kunahusisha dhana nzuri za watu kuhusu maisha: Je, unao moyo unaompenda Mungu? Kina cha yale umeyapitia ulipotembea kwenye njia hii ni kipi? Upendo wako wa Mungu ni safi vipi? Kutenda kwako ukweli ni sahihi vipi? Ili kufanywa kuwa mkamilifu, lazima mtu awe na maarifa ya kimsingi ya vipengele vyote vya ubinadamu. Hili ni hitaji la kimsingi. Wale wote wasioweza kufanywa kuwa wakamilifu baada ya kushindwa hugeuka na kuwa vyombo vya huduma na hatimaye bado watatupwa kwenye ziwa la moto na kibiriti na bado wataanguka ndani ya shimo lisilokuwa na mwisho kwa sababu ya tabia yao ambayo haijabadilika na wangali ni wa Shetani. Mtu akikosa sifa za kukamilishwa, basi yeye ni bure—hana manufaa, ni chombo, kitu ambacho hakiwezi kustahimili majaribio ya moto! Upendo wako wa Mungu sasa hivi ni mkubwa kiasi gani? Chuki yako kwako ni kubwa kiasi gani? Je, kweli unamjua Shetani kwa kina kiasi gani? Umekaza uamuzi wenu? Maisha yako katika ubinadamu yamethibitiwa vyema? Maisha yako yamebadilika? Unayaishi maisha mapya? Mtazamo wenu wa maisha umebadilika? Kama mambo haya hayajabadilika, huwezi kufanywa kuwa mkamilifu hata kama hurudi nyuma; badala yake, wewe umeshindwa tu. Wakati ukifika wa kukujaribu, unakosa ukweli, ubinadamu wako si wa kawaida, na wewe ni wa kiwango cha chini kama mnyama. Umeshindwa tu, umekuwa tu mtu aliyeshindwa tu na Mimi. Kama vile tu, punde punda anapopitia mjeledi wa bwana wake, yeye huwa na woga na hofu ya kufanya chochote kila wakati anapomwona bwana wake, ndivyo pia wewe ulivyo kama punda huyo aliyedhibitiwa. Kama mtu anakosa vipengele hivyo vizuri na badala yake yeye ni wa kutoonyesha hisia na mwenye woga, mwepesi kutishwa na wa kusitasita katika mambo yote, asiyeweza kutambua chochote kwa njia iliyo wazi, asiyeweza kukubali ukweli, ambaye bado hana njia ya kutendea, na hata zaidi asiye na moyo wa upendo wa Mungu—kama mtu hana uelewa wa namna ya kumpenda Mungu, namna ya kuishi maisha yenye maana, au namna ya kuwa mtu halisi—mtu kama huyu anawezaje kumshuhudia Mungu? Hii inaonyesha kwamba maisha yako yanayo thamani ndogo na wewe si

kingine ila punda aliyedhibitiwa. Wewe umeshindwa, lakini hilo linamaanisha tu kwamba umelikataa lile joka kubwa jekundu na umekataa kumilikiwa nalo; hiyo inamaanisha kwamba wewe unaamini kuwa kunaye Mungu, unataka kutii mipango yote ya Mungu na huna malalamiko yoyote. Lakini je, katika vipengele vyema, unaweza kuishi kwa kudhihirisha neno la Mungu na kumbainisha Mungu? Ikiwa huna lolote kati ya haya, inamaanisha kwamba hujamilikiwa na Mungu, na kwamba wewe ni punda aliyedhibitiwa tu. Hakuna chochote cha kutamanika ndani yako, na Roho Mtakatifu hayumo kazini ndani yako. Ubinadamu wako unakosa mengi na haiwezekani Mungu kukutumia. Lazima uidhinishwe na Mungu na kuwa bora zaidi mara mia moja kuliko wanyama wasioamini na kuliko wanaotembea wakiwa wafu—wale tu wanaofikia kiwango hiki ndio wanaostahili kufanywa kuwa wakamilifu. Ni iwapo tu mtu anao ubinadamu na dhamiri ndio anafaa kutumiwa na Mungu. Ni wakati tu ambapo mnakamilishwa ndio mnaweza kufikiriwa kuwa binadamu. Wale waliofanywa kuwa wakamilifu tu ndio wale wanaoishi maisha yenye maana. Watu kama hawa tu ndio wanaoweza kumshuhudia Mungu hata pakubwa.

Mnapaswa Kuweka Pembeni Baraka za Hadhi na Kuelewa Mapenzi ya Mungu ya Kumletea Mwanadamu Wokovu

Kwa mwanadamu, haiwezekani kwa wana wa Moabu kuwa wakamilifu na hawajahitimu kufanywa hivyo. Wana wa Daudi, kwa upande mwingine, hakika wana matumaini na hakika wanaweza kufanywa kamili. Kwa sharti kwamba mtu ni mzawa wa Moabu, basi hawezi kufanywa kamili. Hata leo, bado hamjui umuhimu wa kazi inayofanyika miongoni mwenu; mpaka katika hatua hii ya sasa bado mnashikilia matumaini yenu ya baadaye katika mioyo yenu na hamtaki kuyaacha. Hakuna mtu anayejali ni kwa nini leo Mungu amewachagua tu—kikundi kisichostahili mno—kukifanyia kazi, hivyo je, kazi hii inafanywa vibaya? Je, hii ni kazi ya uangalizi wa muda mfupi? Kwa nini Mungu ameshuka chini bila upendeleo kufanya kazi kati yenu, ingawaje Amekuwa akijua kwa muda mrefu kwamba nyinyi ni wana wa Moabu? Je, hamfikiri kuhusu jambo hili asilani? Je, Mungu hafikirii kamwe juu ya hili Anapofanya kazi Yake? Je, Yeye hutenda kwa ujeuri? Je, Hakujua kwamba ninyi ni wana wa Moabu tangu mwanzo? Je, hamjui kuzingatia mambo haya? Je, “dhana” zenu zimekwenda wapi? Je, mawazo yenu maridhawa yamerekebishwa visivyo? Je, ustadi wenu na hekima yenu zimekwenda wapi? Je, ni kwamba mna ujeuri kama huu wa ajabu ndiyo hamjali jambo kama hilo? Mawazo yenu yana wepesi sana wa kuona kwa mambo kama matarajio yenu ya baadaye na hatima yenu wenyewe, lakini juu ya chochote kingine hayajali na ni yenye upumbavu na ujinga kabisa. Ni nini sasa mnayoamini? Matumaini yenu ya baadaye? Au Mungu? Je, si wewe unaamini tu hatima yako nzuri? Matarajio yako ya baadaye tu? Je, unaelewa kiasi kipi kuhusu njia ya

maisha? Je, umefikia kiasi gani? Je! unafikiri kwamba kazi inayofanyika sasa juu ya wana wa Moabu inafanywa ili kukufedhehesha? Je, inafanywa kimakusudi ili kufichua ubaya wenu? Je, inafanywa kimakusudi ili kuwafanya ninyi kukubali kuadibu na kisha kuwatupa katika ziwa la moto? Sijawahi kusema kuwa hamkuwa na mategemeo, sembuse kwamba mlipaswa kuangamizwa au kupotea; je, Nimetangaza hadharani jambo hilo? Wewe husema kuwa huna tumaini, lakini si hili ni hitimisho lako? Je, si hii ni athari ya mawazo yako mwenyewe? Je, hitimisho lako lina maana? Nikisema wewe hujabarikiwa basi utakuwa kitu cha kuharibiwa, na Nikisema umebarikiwa basi wewe hakika hutaangamizwa. Ninasema sasa tu kwamba wewe ni mzao wa Moabu. Sikusema kuwa wewe utaharibiwa. Ni kwamba tu wana wa Moabu wamelaaniwa, na ni aina moja ya wanadamu waliopotoshwa. Dhambi zimerejelewa awali; Je, si nyinyi nyote ni wenye dhambi? Je, wenye dhambi wote si wamepotoshwa na Shetani? Je, wenye dhambi wote si wanakosa kutii na wanaasi dhidi ya Mungu? Je, wale wanaomdharau Mwenyezi Mungu sio vitu vya laana? Lazima wenye dhambi wote wasiangamizwe? Katika hali hiyo, ni nani kati ya wale wa mwili na damu anayeweza kuokolewa? Mnawezaje kuwa mmeokoka mpaka leo? Ninyi ni wabaya kwa sababu ninyi ni wana wa Moabu, na je, ninyi pia si wanadamu, wenye dhambi? Je, mmedumu vipi hadi leo? Ukamilifu unapotajwa mnakuwa na furaha. Mmesikia kwamba mnapaswa kupitia shida kubwa, na mnafikiri kuwa hili limebarikiwa hata zaidi. Mnafikiri kuwa kwa njia ya dhiki mnaweza kuwa washindi, na hii ni zaidi ya baraka kubwa ya Mungu na furaha yake kuu kwenu. Moabu anaporejelewa, mshtuko unatokea kati yenu. Watu wazima na watoto pia huhisi huzuni isiyoelezeka na mioyo yenu inajaa dhiki; ninyi nyote mnajuta kuzaliwa. Hamwelewi umuhimu wa kwa nini hatua hii ya kazi inafanywa kwa wana wa Moabu; mnajua tu kutafuta hadhi ya juu, na mnarudi nyuma mnapofikiria kuwa hamna tumaini. Ukamilifu na hatima ya baadaye vinapotajwa, mnahisi furaha. Imani yenu kwa Mungu ni ili kupata baraka, na ili muwe na hatima nzuri. Watu wengine sasa wanahisi wasiwasi kwa sababu ya hadhi zao. Kwa sababu wana thamani ya chini, na hali ya chini, basi hawataki kutafuta kukamilishwa. Mungu kwanza alizungumza juu ya ukamilifu, kisha baadaye Akarejelea wazao wa Moabu, kwa hivyo watu walikana njia ya ukamilifu iliyotaja hapo awali. Hii ni kwa sababu hamjawahi kutambua umuhimu wa kazi hii, wala hamjali juu ya umuhimu wake. Vimo vyenu ni vidogo sana na hamuwezi hata kuvumilia usumbufu kidogo. Mnapoona kwamba hali yenu wenyewe ni duni sana mnahisi hasi, na hamna imani ya kuendelea kutafuta. Watu huona tu kupata neema na furaha ya amani kama ishara ya imani katika Mungu, na kutafuta baraka kama msingi wa imani katika Mungu. Watu wachache sana wanatafuta kumjua Mungu au kutafuta mabadiliko katika tabia zao. Imani ya watu katika Mungu hutafuta kumfanya Mungu kuwapa hatima inayofaa, kuwapa neema yote chini ya jua, kumfanya Mungu mtumishi wao, kumfanya Mungu adumishe uhusiano wa amani, wa kirafiki pamoja nao, na ili kusiwe na mgogoro wowote kati yao. Yaani, imani yao kwa Mungu inahitaji Mungu kutoa ahadi ya kutimiza mahitaji yao

yote, kuwapa chochote wanachoomba, kama ambavyo inasema katika Biblia “Nitazisikiliza sala zenu zote.” Wanahitaji Mungu kutomhukumu mtu yeyote au kushughulika na mtu yeyote, kwa kuwa Mungu daima ni Mwokozi Yesu mkarimu, ambaye huwa na uhusiano mzuri na watu wakati wote na mahali pote. Hivi ndivyo watu wanavyomwamini Mungu: Wao wanafanya madai kwa Mungu bila haya, wakiamini kwamba wawe ni waasi au watiifu, Atawapa tu kila kitu bila kufikiri. Wao daima “wanadai madeni” kutoka kwa Mungu, wakiamini kwamba lazima “Awalipe” bila upinzani wowote na, aidha, Alipe mara dufu; wanafikiri, Mungu awe amepata chochote kutoka kwao au la, Anaweza tu kuwa chini yao; Hawezi kuwapanga watu kiholela, sembuse Hawezi kuwafunulia watu hekima Yake ya kale ya siri na tabia ya haki kama Anavyotaka, bila ruhusa yao. Wao huungama tu dhambi zao kwa Mungu wakiamini kwamba Mungu atawasamehe tu, kwamba Hawezi kuchoshwa na kufanya hilo, na kwamba hili litaendelea milele. Wanamwamuru Mungu wapendavyo tu, wakiamini kwamba Yeye atawatii tu, kwa sababu imerekodiwa katika Biblia kwamba Mungu hakuja kutumikiwa na wanadamu, ila kuwatumikia, na kwamba Alikuwa kuwa mtumishi wa mwanadamu. Je, si siku zote mmeamini kwa njia hii? Wakati ambapo hamuwezi kupata chochote kutoka kwa Mungu basi mnataka kukimbia. Na wakati ambapo hamuelewi kitu mnapata hasira, na hata kwenda mbali ili kutoa aina zote za matusi. Hamuwezi tu kumruhusu Mungu Mwenyewe kuonyesha kikamilifu hekima na shani Yake, lakini badala yake unataka tu kufurahia urahisi wa muda na faraja. Hadi sasa, mtazamo wenu katika imani yenu kwa Mungu umekuwa sawa na maoni ya zamani. Mungu akiwaonyesha utukufu mdogo tu mnakosa furaha; je, mnaona sasa jinsi kimo chenu kilivyo? Msifikiri kuwa ninyi nyote ni waaminifu kwa Mungu wakati kwa kweli maoni yenu ya zamani hayajabadilika. Wakati ambapo hakuna chochote kibaya kinachokuangukia, unafikiri kwamba kila kitu kinaelekea kwa urahisi na unampenda Mungu kwa vilele vya juu zaidi. Lakini kitu kidogo kinapokukumba, unakushuka kuzimuni. Je, huku ni wewe kuwa mwaminifu kwa Mungu?

Kama hatua ya mwisho ya kazi ya ushindi ingeanzia Israeli, basi kazi ya ushindi isingekuwa na maana. Kazi ni ya umuhimu zaidi wakati ikiwa inafanyika nchini humu, inapofanyika kwenu enyi watu. Ninyi ni watu wanyenyekevu zaidi, watu walio na hadhi ndogo zaidi. Ninyi ni watu katika ngazi ya chini kabisa ya jamii hii na ninyi ndio ambao walimtambua Mungu kwa kiwango cha chini sana mwanzoni. Ninyi ni watu ambao wamekwenda mbali zaidi na Mungu, na ni wale ambao wamejeruhiwa vibaya. Kwa sababu hatua hii ya kazi ni kwa ajili tu ya ushindi, je, haifai zaidi kuwachagua kuwa na ushuhuda ujao? Ikiwa hatua ya kwanza ya kazi ya ushindi haikufanyika kwenu, basi itakuwa vigumu kuendeleza kazi ya kushinda inayokuja, kwa sababu kazi ya ushindi ambayo itafuatia itafikia matokeo kulingana na ukweli kuwa hii Kazi inafanyika leo. Kazi ya ushindi leo ni mwanzo tu wa kazi nzima ya ushindi. Ninyi ni kundi la kwanza kushindwa; ninyi ni wawakilishi wa wanadamu wote ambao wanashindwa. Ikiwa kuna mtu

yeyote aliye na ufahamu kweli, ataona kwamba kazi yote ambayo Mungu anafanya leo ni kubwa, kwamba Mungu hawaruhusu tu watu kujua uasi wao wenyewe, Yeye pia hufunua hali zenu. Madhumuni na maana ya maneno Yake sio kuwafanya watu kuwa wabaya, wala sio kusababisha watu kuanguka chini. Ni ili kwamba waweze kupata ufunuo na kuokolewa kupitia maneno Yake; ni kufufua roho ya mwanadamu kupitia maneno Yake. Kutoka wakati wa uumbaji wa dunia mpaka sasa, mwanadamu daima ameishi chini ya utawala wa Shetani, bila kujua kwamba kuna Mungu na kutoamini kuna Mungu. Kwamba watu hawa wanaweza kuingizwa katika wokovu mkuu wa Mungu na kuinuliwa sana na Mungu kwa kweli inaonyesha upendo wa Mungu; wale wanaoelewa kweli wote watafikiria kwa njia hii. Je, watu hao wasio na ufahamu watafikiria vipi? “Ah, Mungu anasema sisi ni uzao wa Moabu. Alisema Mwenyewe kuwa sisi ni wana wa Moabu. Je, tunaweza kuwa wazuri? Ni nani aliyetufanya sisi kuwa wana wa Moabu? Ni nani ambaye alitufanya hapo awali kumuasi Yeye sana? Mungu amekuja kutuhukumu; je, huoni jinsi Mungu alivyotuhukumu daima tangu mwanzo? Kwa kuwa tumemkataa Mungu tunapaswa kuadibiwa kwa njia hii.” Je, maneno haya ni sahihi? Leo Mungu anawahukumu, na kuwadibu, na kuwashutumu, lakini jueni kwamba shutuma yako ni ili kukufanya kuweza kujijua. Shutuma, laana, hukumu, kuadibu—haya yote ni ili kwamba uweze kujijua, ili tabia yako iweze kubadilika, na, zaidi ya hayo, ili uweze kujua thamani yako, na kutambua kwamba vitendo vyote vya Mungu ni vyenye haki, na kulingana na tabia Yake na mahitaji ya kazi Yake, kwamba Anafanya kazi kulingana na mpango Wake kwa wokovu wa mwanadamu, na kwamba Yeye ndiye Mungu mwenye haki anayempenda mwanadamu, na kumwokoa mwanadamu, na Anayemhukumu na kumwadibu mwanadamu. Kama utajua tu kwamba wewe ni mwenye hadhi ya chini, kwamba umepotoka na hutii, lakini hujui kwamba Mungu angependa kuweka wazi wokovu Wake kupitia kwa hukumu na kuadibu ambako Anafanya ndani yako leo, basi huna njia yoyote ya kupitia haya, isitoshe huwezi kuendelea mbele. Mungu hajaja kuua, au kuangamiza, lakini kuhukumu, kulaani, kuadibu, na kuokoa. Kabla ya hitimisho ya mpango Wake wa usimamizi wa miaka 6,000—kabla ya Yeye kuweka wazi mwisho wa kila aina ya binadamu—kazi ya Mungu ulimwenguni utakuwa kwa ajili ya wokovu, yote haya ni ili kuwafanya wale wanaompenda Yeye kukamilika kabisa, na kuwarejesha katika utawala Wake. Bila kujali jinsi ambavyo Mungu huwaokoa watu, yote hufanywa kwa kuwafanya wajitenge na asili yao ya zamani ya kishetani; yaani, Yeye huwaokoa kwa kuwafanya watafute uzima. Wasipotafuta uzima basi hawatakuwa na njia yoyote ya kukubali wokovu wa Mungu. Wokovu ni kazi ya Mungu Mwenyewe na kutafuta uzima ni kitu ambacho mwanadamu anapaswa kumiliki ili kupokea wokovu. Kwenye macho ya mwanadamu, wokovu ni upendo wa Mungu, na upendo wa Mungu hauwezi kuwa kuadibu, kuhukumu, na kulaani; wokovu lazima uwe na upendo, huruma, na, zaidi ya hayo, maneno ya faraja, na lazima wokovu uwe na baraka zisizo na mipaka kutoka kwa Mungu. Watu husadiki kwamba wakati Mungu anapomwokoa mwanadamu Anafanya hivyo

kwa kumgusa kwa baraka na neema Zake, ili kwamba waweze kumpa Mungu mioyo yao. Hivyo ni kusema, Yeye kumgusa mwanadamu ni kumwokoa. Aina hii ya wokovu inafanywa kwa kufanya makubaliano. Pale tu ambapo Mungu atampa yeye mara mia ndipo mwanadamu atatiimbele ya jina la Mungu, na kulenga kuwa na mienendo mizuri mbele ya Mungu na kumletea Yeye utukufu. Haya si mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu. Mungu amekuja kufanya kazi ulimwenguni ili kumwokoa mwanadamu aliyepotoka—hakuna uongo katika haya; kama upo, Asingefanya kazi Yake yeye Mwenyewe. Kitambo, mbinu Zake za wokovu zilikuwa kuonyesha upendo na huruma mkuu, kiasi cha kwamba Alijitolea Yake yote kwa Shetani ili naye aweze kuwapata wanadamu wote. Leo haifanani kamwe na kitambo: Wokovu uliopewa leo unatokea wakati wa siku za mwisho, wakati wa uainishaji wa kila mmoja kulingana na aina yake; mbinu za wokovu wako si upendo wala huruma, lakini kuadibu na hukumu ili mwanadamu aweze kuokolewa kabisa. Hivyo basi, kila kitu unachopokea ni kuadibu, hukumu, na kupiga bila huruma, lakini jua kwamba katika kupiga huku kusiko na huruma hakuna hata adhabu ndogo zaidi, jua kwamba licha ya namna ambavyo maneno haya yanavyoweza kuwa makali, kile kinachokupata ni maneno machache yanayoonekana kutokuwa na huruma kabisa kwako, na jua kwamba, licha ya namna ambavyo hasira Yangu itakavyokuwa, kile kitakachokujia bado ni maneno ya mafunzo, na sinui kukudhuru, au kukuua. Je, haya yote ni ukweli, sivyo? Jua kwamba leo, iwe hukumu ya haki au usafishaji na adhabu visivyo na huruma, yote haya ni kwa minajili ya wokovu. Haijalishi kama leo kila anaainishwa kulingana na aina yake, ama makundi ya wanadamu yanafichuliwa, matamko yote ya Mungu na kazi ni kwa ajili ya kuwaokoa wale wanaompenda Mungu kwa dhati. Kuhukumu kwa haki ni kwa ajili ya kumtakasa mwanadamu, utakasaji usio na huruma ni kwa ajili ya kumsafisha mwanadamu, maneno makali au kuadibu yote ni kwa ajili ya kutakasa, na kwa minajili ya wokovu. Na hivyo, mbinu ya leo ya wokovu haifanani na ya kitambo. Leo, kuhukumu kwa haki kunakuokoa wewe, na ni zana nzuri pia ya kumuainisha kila mmoja wenu kulingana na aina, na kuadibu kusiko na huruma kunawaletea wokovu mkubwa—na ni kipi ambacho unahitajika kusema mbele ya kuadibu na kuhukumu huku? Je, hujafurahia wokovu kutoka mwanzo hadi mwisho? Nyote mmeona Mungu mwenye mwili na kutambua kudura na hekima Yake; zaidi ya hayo, umepitia hali ya kupigwa na kufundishwa nidhamu mara kwa mara. Lakini je, hujapokea pia neema kubwa? Je, baraka zako si kubwa zaidi kuliko za mtu yeyote mwingine? Neema zako ni nyingi zaidi kuliko utukufu na utajiri uliofurahiwa na Sulemani! Hebu fikiria: Kama nia Yangu ya kuja ulimwenguni ingekuwa ni kushutumu na kukuadhibu wewe, na wala si kukuokoa, je, siku zako zingedumu kwa muda mrefu? Mngeweza, enyi viumbe wenye dhambi wa mwili na damu, kuishi hadi leo? Kama ingekuwa tu ni kwa ajili ya kuwaadhibu nyinyi, kwa nini Nikawa mwili na kuanza kushughulikia shughuli kubwa kama hiyo? Je, kuwaadhibu ninyi wanadamu wa kufa hakuwezi kufanywa kwa kutamka neon moja tu? Ngingekuwa bado na haja ya kuwaangamiza baada ya kuwashutumu kwa

makusudi? Je, bado hamwamini haya maneno Yangu? Ningeweza kumwokoia mwanadamu kupitia tu kwa upendo na huruma? Au Ningetumia tu kusulubishwa kwa minajili ya kumwokoia mwanadamu? Je, tabia Yangu yenye haki si nzuri zaidi ya kumfanya mwanadamu kuwa mtiifu kabisa? Je, haiwezi kabisa kumwokoia mwanadamu zaidi?

Ingawa maneno Yangu yanaweza kuwa makali, yote yanasemwa kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu, kwa kuwa Ninazungumza tu maneno na sio kuuadhibu mwili wa mwanadamu. Maneno haya humsababisha mwanadamu kuishi katika nuru, kujua kwamba mwanga upo, kujua kwamba mwanga ni wa thamani, hata zaidi kujua jinsi maneno haya yalivyo na manufaa kwa mtu, na kujua kwamba Mungu ni wokovu. Ingawa Nimesema maneno mengi ya kuadibu na hukumu, hayajafanywa kwako katika vitendo. Nimekuja kufanya kazi Yangu, kuzungumza maneno Yangu na, ingawa maneno Yangu yanaweza kuwa magumu, yanasemwa kwa hukumu ya upotovu na uasi wako. Madhumuni Yangu ya kufanya hili yanabaki kumwokoia mtu kutoka kwa utawala wa Shetani, kutumia maneno Yangu ili kumwokoia mwanadamu; Kusudi Langu sio kumdhuru mwanadamu kwa maneno Yangu. Maneno Yangu ni makali ili matokeo yaweze kupatikana kutoka katika Kazi Yangu. Ni katika kufanya kazi kwa njia hii tu ndipo mtu anaweza kujijua na anaweza kujitenga mbali na tabia yake ya uasi. Umuhimu mkubwa zaidi wa kazi ya maneno ni kuwaruhusu watu kuweza kutia katika matendo ukweli baada ya kuuelewa ukweli, kutimiza mabadiliko katika tabia yao, na kutimiza maarifa kuhusu wao wenyewe na kazi ya Mungu. Mbinu za kufanya kazi tu kupitia kwa kuongea ndizo zinazoweza kuleta mawasiliano kuhusu uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu, maneno tu ndiyo yanayoweza kuelezea ukweli. Kufanya kazi kwa njia hii ndiyo mbinu bora zaidi ya kumshinda mwanadamu; mbali na matamko ya maneno, hakuna mbinu nyingine inayoweza kumpatia mwanadamu uelewa wa wazi zaidi wa ukweli na kazi ya Mungu, na hivyo basi katika awamu Yake ya mwisho ya kazi, Mungu anazungumza naye mwanadamu ili kuweza kuwa wazi kwa mwanadamu kuhusu ukweli na siri zote ambazo haelewi, na hivyo basi kumruhusu kufaidi njia ya kweli na uzima kutoka kwa Mungu na kisha kutosheleza mapenzi ya Mungu. Madhumuni ya kazi ya Mungu juu ya mwanadamu ni ili aweze kukidhi mapenzi ya Mungu na yote yamefanywa kumwokoia mwanadamu, kwa hivyo wakati wa wokovu wake wa mwanadamu Yeye hafanyi kazi ya kumwadibu mtu. Wakati wa wokovu wa mwanadamu, Mungu haadhibu maovu au kulipa mema, wala Yeye hafunui hatima ya aina zote za watu. Badala yake, ni baada tu ya hatua ya mwisho ya kazi Yake kukamilishwa ndipo basi Atafanya kazi ya kuadhibu maovu na kulipa mazuri, na kisha basi ndipo Atafunua mwisho wa aina zote za watu. Wale ambao wanaadhibiwa hakika hawataweza kuokolewa, wakati wale waliookolewa watakuwa wale ambao wamepata wokovu wa Mungu wakati wa wokovu Wake wa mwanadamu. Wakati wa kazi ya Mungu ya wokovu, wale wote ambao wanaweza kuokolewa wataokolewa kwa upeo wa juu zaidi, hakuna hata

mmoja wao atakayeachwa, kwa kuwa kusudi la kazi ya Mungu ni kumwokoa mwanadamu. Wote ambao, wakati wa wokovu wa Mungu wa mwanadamu, hawawezi kufikia mabadiliko katika tabia zao, wote ambao hawawezi kumtii Mungu kabisa, wote watakuwa walengwa wa adhabu. Hatua hii ya kazi—kazi ya maneno—humwekea wazi mwanadamu njia na siri zote ambazo haelewi, ili mwanadamu aweze kuelewa mapenzi ya Mungu na mahitaji ya Mungu kwa mwanadamu, ili aweze kuwa katika ile hali ya kutia katika matendo maneno ya Mungu na kutimiza mabadiliko hayo katika tabia yake. Mungu huyatumia maneno tu kufanya kazi Yake, na hawaadhibu watu kwa sababu ni waasi kidogo, kwa sababu sasa ndio wakati wa kazi ya wokovu. Kama kila mtu ambaye alikuwa muasi angeadhibiwa, basi hakuna mtu ambaye angepata fursa ya kuokolewa; wote wangeadhibiwa na kuanguka kuzimuni. Kusudi la maneno ya yanayomhukumu mtu ni kumwezesha kujitambua na kumtii Mungu; sio kwao kuadhibiwa kwa njia ya hukumu ya maneno. Wakati wa kazi ya maneno, watu wengi watafunua uasi wao na kutotii kwao, na wataweka wazi kutotii kwao kwa Mungu mwenye mwili. Lakini Yeye hatawaadhibu watu hawa wote kwa sababu ya hili, badala yake Atawatupa kando wale ambao wamepotoka kabisa na ambao hawawezi kuokolewa. Atautoa mwili wao kwa Shetani, na katika hali kadhaa, kumaliza mwili wao. Wale ambao wanaachwa wataendelea kufuata na kupitia kushughulikiwa na kupogolewa. Ikiwa wanapofuata hawawezi kukubali kushughulikiwa na kupogolewa na wanazidi kupotoka, basi watu hawa watapoteza nafasi zao za wokovu. Kila mtu ambaye amekubali ushindi wa maneno atakuwa na nafasi nzuri ya wokovu. Wokovu wa Mungu wa kila mmoja wa watu hawa huwaonyesha upole Wake mkubwa, kumaanisha kwamba wanaonyeshwa uvumilivu mkubwa. Mradi watu warudi kutokakatika njia mbaya, mradi kama waweze kutubu, basi Mungu atawapa fursa ya kupata wokovu wake. Watu wanapoasi dhidi ya Mungu kwanza, Mungu hana hamu ya kuwaua, lakini badala yake Anafanya yote Anayoweza kuwaokoa. Ikiwa mtu kwa kweli hana nafasi ya wokovu, basi Mungu atamtupa pembeni. Kwamba Mungu si mwepesi wa kumwadhibu mtu ni kwa sababu Anataka kuwaokoa wale wote ambao wanaweza kuokolewa. Yeye huwahukumu, huwapa nuru na kuwaongoza watu tu kwa maneno, na Hatumii fimbo kuwaua. Kutumia maneno kuwaokoa watu ni kusudi na umuhimu wa hatua ya mwisho ya kazi.

Ni Jinsi Gani Ambavyo Mwanadamu Ambaye Amemwekea Mungu Mipaka katika Fikiria Zake Anaweza Kupokea Ufunuo wa Mungu?

Kazi ya Mungu inaendelea kusonga mbele, na ingawa madhumuni ya kazi Yake bado hayajabadilika, njia anazozitumia kufanya kazi zinabadilika mara kwa mara, na hivyo pia wale wanaomfuata Mungu. Zaidi iwapo kazi ya Mungu, zaidi mwanadamu anakuja kumjua kwa kina

Mungu, na tabia ya mwanadamu inabadilika ipasavyo pamoja na kazi Yake. Hata hivyo, ni kwa sababu kazi ya Mungu milele inabadilika ndio wale wasiojua kazi ya Roho Mtakatifu na wale wanadamu wajinga wasiojua ukweli wanakuwa wapinzani wa Mungu. Kazi ya Mungu kamwe haifuati dhana za mwanadamu, kwani kazi Yake daima ni mpya na siyo nzee. Kamwe Hairudii kazi ya zamani lakini badala Anasonga mbele na kazi ambayo haijafanywa hapo awali. Kwa sababu Mungu harudii kazi Yake na mwanadamu daima anahukumu kazi ya Mungu leo kulingana na kazi Yake ya zamani, ni vigumu sana kwa Mungu kutekeleza kila hatua ya kazi ya enzi mpya. Mwanadamu ana vizuizi vingi sana! Kufikiria kwa mwanadamu ni kwa akili finyu! Hakuna mwanadamu anayeijua kazi ya Mungu, lakini bado wote wanafafanua kazi hiyo. Mbali na Mungu, mwanadamu anapoteza uhai, ukweli na baraka za Mungu, lakini bado mwanadamu hajapokea uhai wala ukweli, na hata baraka kubwa Mungu anazowapa wanadamu. Wanadamu wote wanataka kumpata Mungu lakini bado hawawezi kuvumilia mabadiliko yoyote kwa kazi ya Mungu. Wale wasiokubali kazi mpya ya Mungu wanaamini kwamba kazi ya Mungu haibadiliki, na kwamba kazi ya Mungu milele inabakia kusimama. Kwa imani yao, yote yanayohitajika kupata wokovu wa milele kutoka kwa Mungu ni kuhifadhi sheria, na iwapo watatubu na kukiri dhambi zao, dhamira ya Mungu milele itaridhika. Wana maoni kwamba Mungu anaweza tu kuwa Mungu chini ya sheria na Mungu aliyesulubiwa kwa sababu ya mwanadamu; pia ni maoni yao kwamba Mungu hastahili na Hawezi kuzidi kiwango cha Biblia. Ni hasa maoni haya yaliyowafunga imara kwa sheria ya zamani na kuendelea kuwafumba kwa kanuni ngumu. Hata zaidi wanaamini kwamba kazi yoyote ile mpya ya Mungu, ni lazima ithibitishwe na unabii, na kwamba katika kila hatua ya hiyo kazi, wote wanaomfuata na roho ya kweli lazima pia waonyeshwe ufunuo, vinginevyo kazi hiyo haiwezi kuwa ya Mungu. Tayari si kazi rahisi kwa mwanadamu kuja kumjua Mungu. Ikichukuliwa pamoja na moyo wa ujinga wa mwanadamu na asili yake ya kuasi ya kujiona muhimu na kujivunia, basi ni vigumu zaidi kwa mwanadamu kukubali kazi mpya ya Mungu. Mwanadamu haitafiti kazi mpya ya Mungu kwa utunzaji wala haikubali na unyenyekevu; badala yake, mwanadamu anachukua mtazamo wa dharau, kusubiri ufunuo na mwongozo wa Mungu. Hii siyo tabia ya mwanadamu anayeasi dhidi ya na kumpinga Mungu? Ni jinsi gani wanadamu kama hawa wanaweza kupata idhini ya Mungu?

Wakati huo, Yesu alisema kuwa kazi ya Yehova ilikuwa imebaki nyuma kwa Enzi ya Neema, kama Nisemavyo leo kwamba kazi ya Yesu imebaki nyuma. Kama kungekuwa tu na Enzi ya Sheria na siyo Enzi ya Neema, Yesu hangeweza kusulubiwa na hangeweza kuwakomboa wanadamu wote; kungekuwa tu na Enzi ya Sheria, kungekuwa na uwezekano wa mwanadamu kuendelea hadi siku ya leo? Historia inaendelea mbele; historia sio asili ya sheria ya kazi ya Mungu? Hii sio picha ya usimamizi Wake wa mwanadamu ndani ya ulimwengu mzima? Historia inaendelea mbele, na pia kazi ya Mungu, na matakwa ya Mungu yanaendelea kubadilika.

Haingewezekana kwa Mungu kudumisha hatua moja ya kazi kwa miaka elfu sita, kwani kila mwanadamu anajua kwamba Yeye daima ni mpya na kamwe si mzee. Hangeweza kuendelea kuendeleza kazi sawa na kusulubiwa, na mara moja, mara mbili, mara tatu.... kupigwa misumari kwa msalaba. Huu ni mtazamo wa mwanadamu mjinga. Mungu haendelezi kazi sawa, na kazi Yake daima inabadilika na daima ni mpya, jinsi kila siku Nazungumza nanyi maneno mapya na kufanya kazi mpya. Hii ndiyo kazi Ninayofanya, umuhimu wake ukiwa kwa maneno “mpya” na “ajabu.” “Mungu habadiliki, na Mungu daima Atakuwa Mungu”; usemi huu hakika ni ukweli. Kiini cha Mungu hakibadiliki, Mungu daima ni Mungu, na Hawezi kamwe kuwa Shetani, lakini haya hayathibitishi kwamba kazi Yake ni ya daima na kabambe kama kiini Chake. Unatangaza kwamba Mungu yuko hivyo, lakini ni jinsi gani basi unaweza kueleza kwamba Mungu daima ni mpya na kamwe si mzee? Kazi ya Mungu inaendelea kuenea, na mapenzi ya Mungu yanaendelea kujitokeza na kufanywa kujulikana na mwanadamu. Wakati mwanadamu anakuwa na uzoefu wa kazi ya Mungu, tabia yake inaendelea kubadilika, na maarifa yake yanaendelea kubadilika. Basi mabadiliko haya yanatokea wapi? Siyo kwa kazi ya Mungu inayobadilika milele? Kama tabia ya mwanadamu inaweza kubadilika, mbona mwanadamu hawezi kuruhusu kazi Yangu na maneno Yangu pia kuendelea kubadilika? Ni lazima Nikabiliwe na vikwazo vya mwanadamu? Hutegemei tu maneno ya hila?

Kufuata kufufuka kwake, Yesu alijitokeza kwa mitume na kusema, “Nawatumieni ahadi ya Babangu kwenu: lakini ngojeni katika mji wa Yerusalemu, mpaka mjaliwe uwezo kutoka juu.” Je, wajua jinsi maneno haya yalielezwa? Umepewa sasa nguvu Zake? Umeelewa sasa kile kinachoitwa nguvu? Yesu alitangaza kwamba wanadamu wangepewa Roho wa ukweli katika siku za mwisho. Sasa ni siku za mwisho; je, unaelewa jinsi Roho wa ukweli hutamka maneno? Roho wa ukweli huonekana na kufanya kazi wapi? Katika kitabu cha unabii cha nabii Isaya, hakuwahi kutajwa kwamba mtoto anayeitwa Yesu angezaliwa katika enzi ya Agano Jipya; bali kuliandikwa tu kwamba mtoto mchanga wa kiume anayeitwa Imanueli angezaliwa. Mbona hakutaja jina Yesu? Hakuna pahali popote kwa Agano la Kale panapotokea jina hili, hivyo mbona basi mnamwamini Yesu? Hakika hamkumwona Yesu kwa macho yenu kabla kuja kumwamini? Ama mlianza kuamini mlipopata ufunuo? Mungu kweli angewaonyesha neema kama hiyo? Na kuwapa baraka kubwa kama hiyo? Je, ni kwa msingi gani mlimwamini Mungu? Mbona basi hamwamini kwamba Mungu amekuwa mwili siku hii? Mbona mnasema kwamba kukosekana kwa ufunuo kutoka kwa Mungu kunathibitisha kwamba Hajakuwa mwili? Ni lazima Mungu amweleze mwanadamu kabla ya kuanza kazi Yake? Ni lazima apate idhini kutoka kwa mwanadamu? Isaya alitangaza tu kwamba mtoto mchanga wa kiume angezaliwa horini lakini hakutabiri kwamba Maria angejifungua Yesu. Mbona basi mlimwamini Yesu aliyezaliwa na Maria? Hakika imani yenu siyo isiyokuwa na uhakika na mkanganyiko! Wengine wanasema

kwamba jina la Mungu halibadiliki, hivyo, mbona basi jina la Yehova likawa Yesu? Ilitabiriwa kuja kwa Masihi, hivyo mbona basi mwanadamu kwa jina Yesu alikuja? Mbona jina la Mungu lilibadilika? Kazi kama hiyo haikufanyika muda mrefu uliopita? Hawezi Mungu leo kufanya kazi mpya? Kazi ya jana inaweza kubadilishwa, na kazi ya Yesu inaweza kufuata baada ya hiyo ya Yehova. Haiwezi kazi ya Yesu kurithiwa na kazi nyingine? Ikiwa jina la Yehova linaweza kubadilishwa kuwa Yesu, basi jina la Yesu haliwezi kubadilishwa pia? Hakuna jambo lolote hapa lisilo la kawaida; ni kwamba tu watu ni punguani sana. Mungu daima atakuwa Mungu. Bila kujali mabadiliko ya kazi Yake na jina Lake, tabia na maarifa Yake hayabadiliki milele. Ikiwa unaamini kwamba Mungu anaweza tu kuitwa na jina Yesu, basi unajua machache sana. Unathubutu kudai kwamba Yesu milele ni jina la Mungu, kwamba Mungu milele na daima atajulikana kwa jina Yesu, na kwamba haya hayatabadilika? Unathubutu kudai kwa uhakika ni jina la Yesu lililohitimisha Enzi ya Sheria na pia kuhitimisha enzi ya mwisho? Nani anaweza kusema kwamba neema ya Yesu inaweza kuhitimisha enzi? Kama sasa huwezi kujua kweli hizi wazi, hutaweza tu kuhubiri injili, lakini pia wewe mwenyewe huwezi kubaki umesimama. Itakapofika siku ambayo utatatua matatizo yote ya hao watu wa kidini na kukanusha imani zao za uwongo, hiyo itakuwa thibitisho kwamba una hakika kabisa ya hatua hii ya kazi na huna shaka hata kidogo. Ikiwa huwezi kukanusha imani zao za uwongo, basi watakushitaki na kukukashifu. Hii sio aibu?

Wayahudi wa wakati huo wote walisoma kutoka Agano la Kale na walijua unabii wa Isaya kwamba mtoto mchanga wa kiume angezaliwa horini. Mbona basi, na maarifa haya, bado walimtesa Yesu? Hii siyo kwa sababu ya asili yao ya kuasi na kutojua kazi ya Roho Mtakatifu? Wakati huo, Mafarisayo waliamini kwamba kazi ya Yesu ilikuwa tofauti na ile waliyojua ya mtoto mchanga wa kiume aliyetabiriwa; mwanadamu wa leo anamkataa Mungu kwa sababu kazi ya Mungu mwenye mwili haikubaliani na Biblia. Si kiini cha uasi wao dhidi ya Mungu ni moja na sawa? Unaweza kuwa yule ambaye anakubali tu bila swali kazi yote ya Roho Mtakatifu? Kama ni kazi ya Roho Mtakatifu, basi ni mkondo sawa, na unastahili kuukubali bila wasiwasi wowote hata kidogo; hufai ya kuchukua na kuchagua kipi cha kukubali. Ukipata ufahamu zaidi kutoka kwa Mungu na kujitahadhari zaidi Kwake, basi hili silo tendo lisilohitajika? Huna haja kutafuta uthibitisho zaidi kutoka kwa Biblia; iwapo ni ya Roho Mtakatifu huna budi kuikubali, kwani unamwamini Mungu kumfuata Mungu, sio kumchunguza. Hupaswi kutafuta ushuhuda zaidi ili Nionyeshe kwamba Mimi ni Mungu wako. Badala yake, unapaswa kupambanua kama Nina faida kwako; hiyo ndiyo muhimu. Hata kama umegundua ushuhuda usioplingika ndani ya Biblia, haiwezi kukuleta kikamilifu mbele Yangu. Wewe ndiye mmoja anayeishi ndani ya mipaka ya Biblia, na sio mbele Yangu; Biblia haiwezi kukusaidia kunijua, wala haiwezi kuimarisha upendo wako Kwangu. Ingawa Biblia ilitabiri kwamba mtoto mchanga wa kiume

angezaliwa, hakuna yeyote angeweza kuelewa kupitia nani unabii ungetimia, kwani mwanadamu hakujua kazi ya Mungu, na hii ndiyo ilisababisha Mafarisayo kusimama dhidi ya Yesu. Wengine wanajua kwamba kazi Yangu iko katika maslahi ya mwanadamu, lakini bado wanaendelea kuamini kwamba Yesu na Mimi ni viumbe tofauti kabisa visivyopatana. Wakati huo, Yesu alizungumza tu na wanafunzi Wake mfululizo wa mahubiri katika Enzi ya Neema, kama jinsi ya kuweka vitendoni, jinsi ya kukusanyika pamoja, jinsi ya kuuliza kwa maombi, jinsi ya kuwatendea wengine, na mengineyo. Kazi Aliyoifanya ilikuwa hiyo ya Enzi ya Neema, na alielezea tu juu ya jinsi wanafunzi na waliomfuata wanapaswa kuweka vitendoni. Alifanya tu kazi ya Enzi ya Neema na hakuna hata moja ya siku za mwisho. Wakati Yehova aliandika sheria ya Agano la Kale kwa Enzi ya Sheria, mbona basi hakufanya kazi ya Enzi ya Neema? Mbona hakueleza wazi mapema kazi ya Enzi ya Neema? Hii haingekuwa ya manufaa kwa kukubali kwa mwanadamu? Alitabiri tu kwamba mtoto mchanga wa kiume angezaliwa na kuja mamlakani, lakini Hakutekeleza mapema kazi ya Enzi ya Neema. Kazi ya Mungu katika kila enzi ina mipaka ya wazi; Anafanya tu kazi ya enzi ya sasa na Hatekelezi hatua ifuatayo ya kazi mapema. Kwa njia hii tu kazi Yake ya kuwakilisha ya kila enzi inaweza kuletwa mbele. Yesu alizungumzia tu ishara za siku za mwisho, kuhusu jinsi ya kuwa mtulivu na jinsi ya kuokolewa, jinsi ya kutubu na kukiri, na pia jinsi ya kubeba msalaba na kuvumilia mateso; Kamwe hakuzungumza kuhusu jinsi mwanadamu katika siku za mwisho anapaswa kuingia ndani, ama jinsi ya kutafuta kukidhi matakwa ya Mungu. Hasa, haingekuwa tendo la imani ya uwongo kutafuta ndani ya Biblia kazi ya Mungu ya siku za mwisho? Nini unaweza kupambanua tu kwa kushika Biblia kwa mikono yako? Uwe mkalimani wa Biblia ama mhubiri, nani anaweza kujua mbeleni kazi ya leo?

“Yeye ambaye ana sikio, na asikie yale ambayo makanisa yaliambiwa na Roho.” Mmeyesikia sasa maneno ya Roho Mtakatifu? Maneno ya Mungu yamekuja juu yenu. Mnayasikia? Mungu anafanya kazi ya neno katika siku za mwisho, na maneno haya ni yale ya Roho Mtakatifu, kwani Mungu ni Roho Mtakatifu na Anaweza pia kuwa mwili; kwa hivyo, maneno ya Roho Mtakatifu, yalivyosemwa zamani, ni maneno ya Mungu mwenye mwili wa leo. Kuna wanadamu wajinga wanaoamini kwamba maneno ya Roho Mtakatifu yanapaswa kuja chini kutoka mbinguni hadi kwa masikio ya mwanadamu. Yeyote anayefikiria hivi hajui kazi ya Mungu. Kwa kweli, matamshi yaliyosemwa na Roho Mtakatifu ni yale yaliyosemwa na Mungu aliyekuwa mwili. Roho Mtakatifu hawezi kuongea moja kwa moja na mwanadamu, na Yehova hakuongea moja kwa moja na watu, hata kwa Enzi ya Sheria. Si ungekuwa uwezekano wa chini zaidi kwamba Angefanya hivyo kwa enzi ya leo? Kwa Mungu kunena matamshi ili kutekeleza kazi, lazima Awe mwili, la sivyoyake haiwezi kukamilisha malengo Yake. Wanaomkataa Mungu ni wale wasiojua Roho ama kanuni ambazo Mungu hufanya kazi. Wanaoamini kwamba sasa ni enzi ya Roho Mtakatifu lakini bado hawakubali kazi Yake mpya ni wale wanaoishi kwa

imani isiyo dhahiri. Wanadamu kama hawa hawatapokea kamwe kazi ya Roho Mtakatifu. Wale wanaotaka tu Roho Mtakatifu azungumze moja kwa moja na kutekeleza kazi Yake, lakini bado hawakubali maneno ama kazi ya Mungu mwenye mwili, kamwe hawataweza kuchukua hatua katika enzi mpya ama kupokea wokovu kamili kutoka kwa Mungu!

Ni Wale tu Wanaomjua Mungu na Kazi Yake Ndio Wanaoweza Kumridhisha Mungu

Kazi ya Mungu mwenye mwili inajumuisha sehemu mbili. Mara ya kwanza Alipofanyika kuwa mwili, watu hawakumwamini au kumfahamu na wakamsulubisha Yesu msalabani. Mara ya pili, pia, watu pia hawakuamini ndani Yake, wala kumfahamu, na kwa mara nyingine wakamsulubisha Kristo msalabani. Je, mwanadamu si adui wa Mungu? Kama mwanadamu hamjui Yeye, mwanadamu anawezaje kuwa mwandani wa Mungu? Na anawezaje kuwa na sifa za kumshuhudia Mungu? Je, si madai ya kumpenda Mungu, kumtumikia Mungu, kumtukiza Mungu yote ni udanganyifu? Kama unayatoa maisha yako kwa haya mambo yasiyokuwa na uhalisi, yasiyoweza kutekelezeka, huoni kama unafanya kazi bure? Unawezaje kuwa mwandani wa Mungu wakati hujui Mungu ni nani? Kufuatilia kama huko si kusio dhahiri na kwa dhahania? Je, sio kwa udanganyifu? Mtu anawezaje kuwa mwandani wa Mungu? Kuna maana gani kivitendo kuwa mwandani wa Mungu? Je, unaweza kuwa mwandani wa Roho wa Mungu? Je, unaweza kuona jinsi Roho alivyo mkubwa na alivyoinuliwa? Kuwa mwandani wa Mungu asiyeonekana, asiyesikika—hili si jambo lisilo dhahiri na la dhahania? Maana ya utendaji ya kufuatilia huku ni gani? Je, sio udanganyifu mtupu tu? Kile unachokifuatilia ni kuwa mwandani wa Mungu, lakini bado ni mtumwa wa Shetani, maana humfahamu Mungu, na kumfuatilia “Mungu wa vitu vyote,” asiye kuwepo ambaye haonekani, hashikiki, na ni wa dhana zako mwenyewe. Kwa maana isiyo dhahiri, huyo “Mungu” ni Shetani, na kwa uhalisi, ni wewe mwenyewe. Unatafuta kuwa mwandani wako mwenyewe halafu bado unasema unatafuta kuwa mwandani wa Mungu—huko si ni kukufuru? Thamani ya ufutiliaji wa aina hii ni nini? Kama Roho wa Mungu hawezi kuwa mwili, basi kiini cha Mungu ni kitu kisichoonekana, Roho wa uzima asiyesikika, asiye kuwa na umbo, hana vitu vya kushikika, hafikiki na mwanadamu hawezi kumtambua. Mwanadamu anawezaje kuwa mwandani wa Roho asiye kuwa na mwili, wa ajabu na asiye weza kueleweka kama huyu? Huu sio utani? Fikira ya kipuuzi kama hiyo ni batili na haitekelezeki. Mwanadamu aliyeumbwa kwa asili yuko tofauti na Roho wa Mungu, sasa inawezekanaje wawili hawa kuwa wandani? Ikiwa Roho wa Mungu hakutambuliwa katika mwili, ikiwa Mungu hakuwa mwili na kujishusha Mwenyewe kwa kufanyika kiumbe, basi mwanadamu aliyeumbwa asingekuwa na sifa na kuwa na uwezo wa kuwa mwandani Wake, na licha ya wachamungu ambao wanaweza kuwa na nafasi ya kuwa wandani wa Mungu baada ya

Roho zao kuingia mbinguni, watu wengi wasingeweza kuwa wandani wa Roho wa Mungu. Na ikiwa mwanadamu anataka kuwa mwandani wa Mungu mbinguni chini ya uongozi wa Mungu mwenye mwili, je, yeye si mwanadamu mpumbavu kupindukia? Mwanadamu anakuwa tu “mwaminifu” kwa Mungu asiyeonekana, na wala hamzingatii Mungu ambaye hawezi kuonekana, kwa maana ni rahisi sana kumfuata Mungu asiyeonekana—mwanadamu anaweza kufanya hivyo kwa vyovyote apendavyo. Lakini njia ya Mungu anayeonekana si rahisi. Mwanadamu ambaye anamtafuta Mungu asiye dhahiri hakika hawezi kumpata Mungu, maana vitu ambavyo si dhahiri na ni vya dhahania vyote vinafikiriwa na mwanadamu, na ambavyo mwanadamu hawezi kuvipata. Ikiwa Mungu ambaye alikuja kwenu angekuwa Mungu wa kifahari na aliyeinuliwa ambaye angekuwa hafikiki kwenu, sasa mngewezaje kutafuta mapenzi Yake? Na mngewezaje kumfahamu na kumwelewa? Ikiwa angefanya kazi Yake tu, na wala hakuwa na uhusiano na mwanadamu, au hakuwa na ubinadamu wa kawaida na hakuweza kufikiwa na mwanadamu mwenye mwili wa kufa, basi, hata kama Alifanya kazi kubwa kwa ajili yako, lakini hukuweza kuhusiana naye, na hukuweza kumwona, utawezaje kumfahamu? Kama isingekuwa kwa kuchukua mwili wa ubinadamu, mwanadamu asingeweza kumjua Mungu; ni kwa sababu tu ya Mungu mwenye mwili ndiyo mwanadamu amefuzu kuwa mwandani wa Mungu mwenye mwili. Mwanadamu huwa mwandani wa Mungu kwa sababu mwanadamu huhusiana naye, kwa sababu mwanadamu huishi naye na kuambatana naye, na kwa hivyo huja kumjua. Isingekuwa hivyo mwanadamu kumtafuta Mungu si kungekuwa ni bure? Hii ni kusema, si kwa sababu ya kazi ya Mungu ndiyo mwanadamu anaweza kuwa mwandani wa Mungu, bali ni kwa sababu ya uhalisi na ukawaida wa Mungu mwenye mwili. Ni kwa sababu tu Mungu huwa mwili ndiyo mwanadamu huwa na nafasi ya kufanya wajibu wake, na nafasi ya kumwabudu Mungu wa kweli. Je, si huu ni ukweli halisi na unaoweza kutekelezeka? Sasa, bado unatamani kuwa mwandani wa Mungu mbinguni? Ni pale tu ambapo Mungu anajinyenyekeza kwa kiwango fulani, ambavyo ni sawa na kusema, ni pale tu ambapo Mungu anafanyika kuwa mwili, ndipo mwanadamu anaweza kuwa mwandani na msiri Wake. Mungu ni wa Roho: Mwanadamu anawezaje kuwa na sifa ya kuwa mwandani wa Roho huyu, ambaye ameinuliwa sana na asiyeweza kueleweka? Ni pale tu ambapo Roho wa Mungu anaposhuka na kuwa mwili, anakuwa kiumbe anayefanana na mwanadamu, ndipo mwanadamu huweza kuelewa mapenzi Yake na kimsingi kumilikiwa naye. Yeye huzungumza na kufanya kazi katika mwili, hushiriki katika furaha, huzuni, na mateso ya mwanadamu, huishi katika dunia ile ile kama mwanadamu, humlinda mwanadamu, na kumwongoza, na kupitia katika hili humsafisha mwanadamu na kumruhusu mwanadamu kupata wokovu Wake na baraka Zake. Baada ya kuvipata vitu hivi, mwanadamu hupata kuyaelewa mapenzi ya Mungu kwa kweli, na ni hapo tu ndipo anaweza kuwa mwandani wa Mungu. Hii ndiyo inaweza kutekelezeka. Kama Mungu angekuwa haonekani na hashikiki, mwanadamu angewezaje kuwa mwandani Wake? Je, si hili ni fundisho

lililo tupu?

Kutokana na kumwamini Mungu hadi sasa, watu wengi wanaendelea kutafuta kile ambacho ni cha kufikirika na dhahania. Hawana uelewa wa uhalisi wa kazi ya Mungu leo, na bado wanaishi miongoni mwa nyaraka na mafundisho. Aidha, wengi bado hawajaingia katika uhalisi wa mafungu mapya ya maneno kama vile “kizazi kipya cha wale wanaompenda Mungu,” “mwandani wa Mungu,” “kielelezo na mfano wa kuigwa katika upendo wa Mungu,” “mtindo wa Petro”; badala yake yale wanayoyatafuta bado ni ya kufikirika na dhahania, bado wanazunguka katika mafundisho, na hawana ufahamu wa uhalisi wa maneno haya. Roho wa Mungu anapokuwa mwili, unaweza kuona na kuigusa kazi Yake katika mwili. Lakini ikiwa bado huwezi kuwa mwandani Wake, kama bado huwezi kuwa msiri Wake, sasa basi utawezaje kuwa msiri wa Roho wa Mungu? Kama humfahamu Mungu wa leo, unawezaje kuwa mmoja wa kizazi kipya kinachompenda Mungu? Je, hizi si nyaraka na mafundisho yasiyokuwa na maana? Je, unaweza kumwona Roho na kuhisi mapenzi Yake? Si haya ni maneno matupu? Haitoshi wewe kusema tu mafungu ya maneno na maneno haya, wala huwezi kupata kibali cha Mungu kwa ushupavu pekee. Unaridhika kwa kuzungumza maneno haya tu, na unafanya hivyo kwa kuridhisha matamano yako binafsi, kuridhisha mitazamo yako isiyokuwa na uhalisi, na kuridhisha mitazamo na fikira zako binafsi. Kama humfahamu Mungu wa leo, basi, bila kujali kile unachofanya, hutaweza kuuridhisha moyo wa Mungu. Kuwa msiri wa Mungu kuna maana gani? Bado huelewi hili? Kwa kuwa mwandani wa Mungu ni mwanadamu, hivyo Mungu pia ni mwanadamu, yaani, Mungu amekuwa mwili, amekuwa mwanadamu. Ni wale tu walio wa aina moja ndio wanaoweza kuitana wasiri, baada ya hapo ndipo tu ndio wanaweza kuchukuliwa kuwa ni wandani. Kama Mungu angekuwa wa Roho, mwanadamu aliyeumbwa angewezaje kuwa mwandani Wake?

Imani yako kwa Mungu, ufuatiliaji wako wa ukweli, na vile unavyofanya mambo yote yanapaswa kujikita katika ukweli: Kila kitu unachokifanya kinapaswa kiwe kinatekelezeka, na hupaswi kufuatilia vitu vile ambavyo ni vya kinjozi tu. Hakuna maana yoyote katika kufanya vitu namna hii, na, aidha, maisha kama hayo hayana maana. Kwa sababu njia yako na maisha havijengwi katika kitu chochote kile isipokuwa uongo na ulaghai, na hufuati vitu ambavyo vina thamani na maana, kitu pekee unachopata ni fikira za kipuuzi tu na mafundisho ambayo hayana ukweli. Vitu kama hivyo havina uhusiano na maana na thamani ya uwepo wako, na vinaweza tu kukuleta katika ulimwengu ulio tupu. Kwa namna hii, maisha yako yote yatakuwa hayana maana au thamani—na kama hufuatilii maisha yenye maana, basi unaweza kuishi mamia ya miaka na yote hiyo inaweza kuwa haina maana yoyote. Hayo yanawezaje kuitwa maisha ya mwanadamu? Haya hakika si ni maisha ya mnyama? Kwa namna iyo hiyo, kama mtajaribu kufuata njia ya imani katika Mungu, na wala msijaribu kumfuata Mungu anayeweza kuonekana, na badala yake

mumwabudu Mungu asiyeonekana na asiyeshekika, basi si kufuatilia kama huko ni bure? Mwisho wake, ufuatiliaji wako kutakuwa ni anguko kubwa. Kufuatilia kwa aina hiyo kuna manufaa gani kwako? Tatizo kubwa zaidi la mwanadamu ni kwamba anaweza kupenda tu vitu ambavyo hawezi kuviona au kuvigusa, vitu ambavyo ni vya siri kubwa na vya kushangaza, na kwamba haviwezi kufikiwa na mwanadamu na haviwezi kufikiwa na mwanadamu. Kadiri vitu hivi vinavyokuwa si halisi, kadiri vinavyochambuliwa na mwanadamu, ambaye anavifuata bila kujali kitu chochote, na hujaribu kuvipata. Kadiri vinavyokuwa si halisi, ndivyo mwanadamu anavyozidi kuvichunguza na kuvichambua zaidi, hata kwenda kwa kiwango cha kufanya mawazo yake ya kina kuyahusu. Kinyume chake, jinsi vitu vinavyokuwa halisi zaidi, ndivyo mwanadamu anavyozidi kuvipuuzi; huviangalia kwa dhara, na hata huvitweza. Huu hasa si mtazamo weni juu ya kazi halisi Ninayoifanya leo? Kadiri mambo hayo yanavyokuwa halisi, ndivyo unavyozidi kuyadharau. Wala hutengi muda kwa ajili ya kuyachunguza, bali unayapuuzi; unayadharau mambo haya halisi yenye kiwango cha chini, yenye matakwa ya moja kwa moja, na hata unakuwa na fikira nyingi kuhusu Mungu huyu ambaye ni halisi sana, na huwezi tu kuukubali uhalisi na ukawaida Wake. Kwa njia hii, huamini katika hali isiyo dhahiri? Una imani thabiti katika Mungu asiye dhahiri wa wakati uliopita, na wala hupendi kumjua Mungu wa kweli wa leo. Hii si kwa sababu Mungu wa jana na Mungu wa leo wanatoka katika enzi tofauti? Si pia kwa sababu Mungu wa jana ni Mungu wa mbinguni aliyeinuliwa, wakati Mungu wa leo ni mwanadamu mdogo wa duniani? Aidha, si pia kwa sababu Mungu anayeabudiwa na mwanadamu ni yule aliyetokana na dhana zake, wakati Mungu wa leo ni mwili halisi uliotengenezwa duniani? Hata hivyo, si kwa sababu Mungu wa leo ni halisi sana kiasi kwamba mwanadamu hamfuatili? Maana kile ambacho Mungu wa leo anamtaka mwanadamu afanye ni kile ambacho mwanadamu hayupo radhi kabisa kukifanya, na ambacho kinamfanya ahisi aibu. Huku sio kufanya mambo yawe magumu kwa mwanadamu? Je, hili halionyeshi makovu yake hapa? Kwa namna hii, wengi wao ambao hawafuati uhalisi wanakuwa maadui wa Mungu mwenye mwili, wanakuwa wapinga Kristo. Huu si ukweli dhahiri? Hapo zamani, wakati Mungu alikuwa hajawa mwili, inawezekana ulikuwa mtu wa dini, au msahilina. Baada ya Mungu kuwa mwili, wasahilina wengi kama hao waligeuka bila kujua na kuwa wapinga Kristo. Unajua ni nini kinachoendelea hapa? Katika imani yako kwa Mungu, hujikiti katika uhalisi au kuufuatilia ukweli, bali unashikilia sana uongo—je, si hiki ndicho chanzo wazi cha uadui wako na Mungu mwenye mwili? Mungu mwenye mwili anaitwa Kristo, hivyo sio kwamba wote ambao hawamwamini Mungu mwenye mwili ni wapinga Kristo? Je, yule unayemwamini na kumpenda ni huyu Mungu mwenye mwili kweli? Je, kweli ni huyu Mungu aliye hai ambaye ni wa halisi zaidi na ambaye ni wa kawaida kabisa? Malengo ya ufuatiliaji wako, zako ni yapi hasa? Yako mbinguni au duniani? Je, ni dhana au ni ukweli? Je, ni Mungu au ni kiumbe fulani asiye kuwa wa kawaida? Kwa kweli, ukweli ndio halisi zaidi katika methali zote za maisha, na ni mkuu kabisa

kuliko methali hizo miongoni mwa wanadamu wote. Kwa sababu ni matakwa ambayo Mungu anayataka kwa mwanadamu, na ni kazi ambayo inafanywa na Mungu mwenyewe, hivyo inaitwa methali ya maisha. Sio methali iliyoundwa kutoka katika kitu fulani, wala si nukuu maarufu kutoka kwa mtu maarufu; badala yake, ni matamshi kwa mwanadamu kutoka kwa Bwana wa mbingu na nchi na vitu vyote, na sio maneno fulani yaliyotolewa na mwanadamu, bali ni maisha asili ya Mungu. Na hivyo unaitwa ni methali ya juu kabisa kupita methali zote za maisha. Ufuatiliaji wa mwanadamu wa kuweka ukweli katika matendo ni kufanya wajibu wake, yaani, ufuatiliaji wa kukidhi matakwa ya Mungu. Asili ya matakwa haya ni ukweli halisi, badala ya mafundisho yasiyokuwa na maana ambayo hayafikiwi na mwanadamu yeyote. Kama kufuatilia kwako ni mafundisho tu na bila uhalisi wowote, huoni unaasi dhidi ya ukweli? Wewe si mtu anayeushambulia ukweli? Mtu wa namna hiyo anawezaje kufuatilia kumpenda Mungu? Watu ambao hawana uhalisi ni wale ambao wanausaliti ukweli, na wote kwa asili ni waasi!

Haijalishi unavyofuatilia, unapaswa kuelewa kazi ambayo Mungu anaifanya leo, na unapaswa kuelewa umuhimu wa kazi hii. Unapaswa kuelewa na kujua ni kazi gani ambayo Mungu anaileta, Atakapokuja katika siku za mwisho, ni tabia gani Anayoileta, na kile kitakachofanywa kikamilifu kwa mwanadamu. Ikiwa hujui au huielewi kazi ambayo Amekuja kufanya katika mwili, basi unawezaje kufahamu mapenzi Yake, na unawezaje kuwa mwandani Wake? Kwa kweli, kuwa mwandani wa Mungu si vigumu, lakini pia si rahisi. Ikiwa watu wanaweza kuelewa na kutekeleza, basi kuwa isiyo na ugumu; ikiwa watu hawawezi kuelewa vilivyo, basi inakuja kuwa ngumu zaidi, na, zaidi, wanakuwa rahisi kuwa wenye ufuatiliaji wao unawafanya wawe wasio yakini. Ikiwa, katika kumfuatilia Mungu, mwanadamu hana msimamo wake wa kusimamia, na hajui ni ukweli gani anapaswa kuufuata, basi ina maana kwamba hana msingi, na hivyo si rahisi kwake kusimama imara. Leo, kuna wengi ambao hawauielewi ukweli, ambao hawawezi kutofautisha kati ya wema na uovu au kipi cha kupenda na kipi cha kuchukia. Watu kama hawa ni vigumu kusimama imara. Kitu cha msingi katika imani kwa Mungu ni kuwa na uwezo wa kuweka ukweli katika matendo, kujali mapenzi ya Mungu, kujua kazi ya Mungu kwa mwanadamu anapokuja katika mwili na kanuni ambazo kwazo Anazungumza; usifuate wengi, na unapaswa kuwa na kanuni katika kile unachokiingia, na unapaswa kuzishika imara. Kuyashikilia imara mambo ambayo yameangaziwa na Mungu kwako ni msaada kwako. Usipofanya hivyo, leo utakwenda njia moja, kesho utakwenda njia nyingine, na hutapata kitu chochote halisi. Kuwa hivi hakuna manufaa yoyote katika maisha yako. Wale ambao hawauielewi ukweli siku zote wanawafuata wengine. Ikiwa watu wanasema kwamba hii ni kazi ya Roho Mtakatifu, basi, wewe pia utasema ni kazi ya Roho Mtakatifu; ikiwa watu watasema ni kazi ya roho mchafu, basi wewe pia utatilia mashaka, au utasema ni kazi ya roho mchafu. Siku zote unakuwa kama kasuku kwa maneno ya wengine, na huwezi kutofautisha kitu chochote

wewe mwenyewe, wala huwezi kufikiri kwa ajili yako mwenyewe. Huyu ni mtu ambaye hana msimamo, ambaye hana uwezo wa kutofautisha—mtu wa aina hiyo ni masikini asiye na thamani. Wewe siku zote hurudia maneno ya wengine: Leo inasemwa kuwa hii ni kazi ya Roho Mtakatifu, lakini kuna uwezekano siku moja mtu atasema si kazi ya Roho Mtakatifu, na si chochote bali matendo ya mwanadamu—na bado huwezi kuelewa, na utakaposhuhudia watu wengine wanasema hivyo, nawe pia unasema kitu kile kile. Kwa kweli ni kazi ya Roho Mtakatifu, lakini unasema ni kazi ya mwanadamu; hujawa mmoja wa wale wanaoikufuru kazi ya Roho Mtakatifu? Katika hili, hujampinga Mungu kwa sababu huwezi kutofautisha? Nani ajuaye, labda siku moja mtu atatokea na kusema “hii ni kazi ya roho mchafu,” na utakaposikia maneno haya utapotea, na kwa mara nyingine tena unafungwa na maneno ya wengine. Kila wakati mtu anapochochea usumbufu huwezi kusimama katika msimamo wako, na hii ni kwa sababu huna ukweli ndani yako. Kuamini katika Mungu na kutafuta maarifa ya Mungu si jambo rahisi. Hayawezi kupatikana kwa kukusanyika pamoja na kusikiliza mahubiri, na huwezi kukamilishwa kwa kupenda tu. Lazima upitie uzoefu, na ujue, na kuongozwa na kanuni katika matendo yako, na kupata kazi za Roho Mtakatifu. Utakapopitia katika uzoefu, utakuwa na uwezo wa kutofautisha mambo mengi—utakuwa na uwezo wa kutofautisha kati ya mema na mabaya, kati ya haki na uovu, kati ya kile ambacho ni cha mwili na damu na kile ambacho ni cha kweli. Unapaswa kuwa na uwezo wa kutofautisha kati ya mambo haya yote, na kwa kufanya hivyo, haijalishi ni mazingira gani, hutapotea kamwe. Hiki tu ndicho kimo chako halisi.

Kuijua kazi ya Mungu si jambo rahisi. Unapaswa kuwa na viwango na malengo katika utafutaji wako, unapaswa kujua jinsi ya kutafuta njia ya kweli, na jinsi ya kupima kujua kama ni njia ya kweli au si ya kweli, na kama ni kazi ya Mungu au kinyume chake. Kanuni ya msingi kabisa katika kuutafuta ukweli ni nini? Unapaswa kuangalia kama kuna kazi ya Roho Mtakatifu au la kwa njia hii, iwapo maneno haya ni maonyesho ya ukweli, yanamshuhudia nani, na ni kitu gani yanaweza kukupatia. Kutofautisha kati ya njia ya kweli na hizi njia za uongo kunahitaji njia kadhaa za maarifa ya msingi, ya msingi kabisa kati ya zote ni kusema iwapo kuna Kazi ya Roho Mtakatifu au la. Maana kiini cha imani ya mwanadamu katika Mungu ni imani katika Roho Mtakatifu. Hata imani yake katika Mungu mwenye mwili ni kwa sababu mwili huu ni mfano halisi wa Roho wa Mungu, ikiwa na maana kwamba imani hiyo bado ni imani katika Roho. Kuna tofauti kati ya Roho na mwili, lakini kwa kuwa mwili unatokana na Roho, na ndio Neno linakuwa mwili, hivyo kile ambacho mwanadamu anaamini katika ni uungu halisi wa Mungu. Na hivyo, katika kutofautisha kama ni njia sahihi au la, zaidi ya yote unapaswa kuangalia kama kuna kazi ya Roho Mtakatifu, na baada ya hapo unapaswa kuangalia kama kuna ukweli katika njia hii. Ukweli huu ni tabia ya maisha ya ubinadamu wa kawaida, ni sawa na kusema, kile ambacho Mungu alitaka kwa mwanadamu alipomuumba hapo mwanzo, yaani, ubinadamu wote

wa kawaida (ikiwa ni pamoja na hisia za kibinadamu, umaizi, hekima, na maarifa ya msingi ya kuwa mwanadamu). Yaani, unapaswa kuangalia iwapo njia hii inaweza kumpeleka mwanadamu katika maisha ya ubinadamu wa kawaida au la, iwapo ukweli uliozungumzwa unahitajika kulingana na uhalisi wa ubinadamu wa kawaida au la, iwapo ukweli huu ni wa kiutendaji au hali, na iwapo ni wa wakati muafaka au la. Ikiwa kuna ukweli, basi unaweza kumpeleka mwanadamu katika uzoefu wa kawaida na halisi; aidha, mwanadamu anakuwa wa kawaida zaidi, hisia za kawaida za kibinadamu zinakuwa kamili zaidi, maisha ya mwanadamu katika mwili na maisha ya kiroho yanakuwa katika mpangilio mzuri zaidi, na mihemko ya mwanadamu inakuwa ya kawaida kabisa. Hii ni kanuni ya pili. Kuna kanuni nyingine moja zaidi, ambayo ni iwapo watu wana maarifa mengi juu ya Mungu au la, kama unapitia uzoefu wa kazi hiyo na ukweli unaweza kuchochea upendo wa Mungu ndani yao au na kuwasogeza karibu zaidi na Mungu. Katika hili, inaweza kupimwa iwapo ni njia sahihi au la. Kanuni ya msingi ni iwapo njia hii ni ya uhalisi badala ya kuwa ya kimiujiza, na iwapo inaweza kutoa maisha ya mwanadamu. Kama inakubaliana na kanuni hizi, hitimisho linaweza kuwekwa kwamba njia hii ni njia ya kweli. Ninasema maneno haya si kuwafanya mkubali njia nyingine katika uzoefu mtakaoupitia baadaye, wala si utabiri kwamba kutakuwa na kazi ya enzi nyingine mpya hapo baadaye. Ninayasema ili mweze kuwa na uhakika kwamba kazi ya leo ni kazi ya kweli, ili kwamba msiwe na uhakika nusu katika imani yenu katika kazi ya leo na kushindwa kuielewa kwa ndani. Kuna hata watu wengi ambao, licha ya kuwa na uhakika, bado wanafuata kwa mkanganyiko; uhakika kama huo hauna kanuni, na wanapaswa kuondolewa siku moja. Hata wale ambao wapo motomoto katika imani yao wanakuwa na uhakika katika mambo matatu na mambo matano wanakuwa hawana uhakika, kitu kinachoonyesha kuwa hawana msingi. Kwa sababu tabia yenu ni dhaifu sana na msingi wenu hauna kina, hivyo hamna uelewa wa kutofautisha. Mungu harudii kazi Yake, Hafanyi kazi ambayo si halisi, Hamtaki mwanadamu afanye mambo zaidi ya uwezo wake, na Hafanyi kazi ambayo inazidi akili ya mwanadamu. Kazi yote Anayofanya ipo ndani ya mawanda ya akili ya kawaida ya mwanadamu, na haizidi ufahamu wa ubinadamu wa kawaida, na kazi Yake ni kulingana na mahitaji ya kawaida ya mwanadamu. Ikiwa ni kazi ya Roho Mtakatifu, mwanadamu anakuwa wa kawaida zaidi, na ubinadamu wako unakuwa wa kawaida kabisa. Watu wanapata maarifa mengi ya tabia yao potovu ya kishetani, na iliyopotoka, na asili ya mwanadamu, na pia wanapata shauku kubwa ya kuuelewa ukweli. Hiyo ni kusema, maisha ya mwanadamu yanakua zaidi na zaidi, na tabia upotovu ya mwanadamu inakuwa na uwezo wa mabadiliko zaidi na zaidi—yote hiyo ni maana ya Mungu kuwa maisha ya mwanadamu. Kama njia haiwezi kufunua vitu hivyo ambavyo ni asili ya mwanadamu, haiwezi kubadilisha tabia ya mwanadamu, na, zaidi ya hayo, hauwezi kumleta mbele ya Mungu au kumpa ufahamu wa kweli juu ya Mungu, na hata kufanya ubinadamu wake kuwa duni zaidi na hisia zake kuwa si za kawaida zaidi, basi njia hii itakuwa si njia ya kweli, na inaweza kuwa ni kazi ya roho mchafu, au

njia ya zamani. Kwa ufupi, haiwezi kuwa kazi ya sasa ya Roho Mtakatifu. Mmemwamini Mungu kwa miaka yote hii, halafu bado hamna uwezo wa kutofautisha kati ya njia ya kweli na njia ya uongo au kuweza kuitafuta njia ya kweli. Watu wengi hawana haja na masuala haya; wanakwenda tu kule ambako wengi wanakwenda, na wanarudia kile ambacho watu wengi wanasema. Mtu kama huyu anawezaje kuwa mtu anayetafuta njia ya kweli? Na watu kama hao wanaweza kuipata njia ya kweli? Ukielewa kanuni hizi muhimu, basi chochote kitakachotokea hutadanganywa. Leo, ni muhimu sana kwamba mwanadamu awe na uwezo wa kutofautisha mambo; hiki ndicho kinapaswa kuwa katika ubinadamu wa kawaida, na kile ambacho mwanadamu anapaswa kuwa nacho katika uzoefu wake. Ikiwa hata leo, mwanadamu bado hawezi kutofautisha kitu katika ufuataji wake wa ukweli, na hisia zake za kibinadamu bado hazikui, basi mwanadamu ni mpumbavu sana, na njia yake ni makosa na imepotoka. Hakuna tofauti hata ndogo katika maisha yako leo, na ingawa ni ukweli, kama unavyosema, umepata njia ya kweli, ni kweli umeipata? Umeweza kuwa na uwezo wa kutofautisha kitu chochote? Kiini cha njia ya kweli ni nini? Katika njia ya kweli, bado hujapata njia ya kweli, hujapata kitu chochote cha ukweli, yaani, hujapata kile ambacho Mungu anataka kutoka kwako, hivyo hakujawa na tofauti katika upotovu wako. Ukiendelea kufuatilia kwa njia hii, hatimaye utaondolewa. Kwa kuwa umefuata mpaka wa leo, unapaswa uwe na uhakika kwamba njia uliyoichukua ni njia sahihi, na hupaswi kuwa na mashaka sana. Watu wengi siku zote wanakuwa hawana uhakika na wanashindwa kufuatilia ukweli kwa sababu ya masuala fulani madogo madogo. Watu kama hao ni wale ambao hawana ufahamu ya kazi ya Mungu, ni wale ambao wanamfuata Mungu katika mkanganyiko. Watu ambao hawajui kazi ya Mungu hawawezi kuwa wandani Wake, au kuwa na ushuhuda Kwake. Ninawashauri wale ambao wanatafuta tu baraka na kufuata kile ambacho si dhahiri na dhahania wafuatilie ukweli mapema iwezekanavyo, ili kwamba maisha yao yaweze kuwa na maana. Msiendelee kujidanganya tena!

Tofauti Kati ya Huduma ya Mungu Mwenye Mwili na Wajibu wa Mwanadamu

Ni lazima myafahamu maono ya kazi ya Mungu na mpate mwelekeo wa kazi Yake. Huku ni kuingia kwa njia nzuri. Punde unapong'amua ukweli wa maono kwa usahihi, kuingia kwako kutakuwa salama; bila kujali kazi Yake hubadilika kiasi gani, utaendelea kuwa imara moyoni mwako, utakuwa wazi kuhusu maono, na utakuwa na lengo la kuingia na kufuatilia kwako. Kwa njia hiyo, uzoefu na ufahamu ulio ndani yako utakua kwa kina na kutakaswa zaidi. Punde unapong'amua taswira nzima kwa ukamilifu, hutapoteza kitu maishani na hutapotea. Kama hutazijua hatua hizi za kazi, utapata hasara kwa kila mojawapo. Huwezi kugeuka baada ya siku chache tu na hutaweza kuipata njia mwafaka hata katika majuma machache. Je, si hili

linakurudisha nyuma? Kuna zaidi katika kuingia kwa njia nzuri dhahiri na vitendo ambavyo mnapaswa kuving'amua, na vilevile unapaswa kuelewa mambo kadha katika maono ya kazi Yake kama vile umuhimu wa kazi Yake ya ushindi, njia ya kufanywa mkamilifu katika siku za usoni, kinachofaa kupatikana kupitia uzoefu wa majaribu na masaibu, umuhimu wa hukumu na kuadibu, kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu, na kanuni za ukamilifu na ushindi. Huu wote ndio ukweli wa maono. Hayo mengine ni hatua tatu za kazi ya Enzi ya Sheria, Enzi ya Neema na Enzi ya Ufalme pamoja na ushuhuda wa baadaye. Huu pia ni ukweli kuhusiana na maono, na ni wa msingi na muhimu sana pia. Kwa sasa, kuna mengi sana mnayopaswa kuingia kwayo na kutenda, na kwa sasa yana safu nyingi na maelezo ya kina. Kama huna ufahamu wa ukweli huu, ni thibitisho kwamba bado hujaingia. Mara nyingi, ufahamu wa mwanadamu kuhusu ukweli huwa wa juujuu; mwanadamu hushindwa kuweka ukweli wa kimsingi katika vitendo na hajui jinsi ya kushughulikia hata maswala madogo. Sababu ya mwanadamu kushindwa kutenda ukweli ni tabia yake ya uasi, na kwa sababu ufahamu wake kuhusu kazi ya sasa ni wa juu juu na wa kuegemea upande mmoja. Kwa hivyo, si kazi rahisi kwa mwanadamu kufanywa mkamilifu. Uasi wako ni wa hali ya juu sana, na unashikilia sana hali yako ya zamani; huwezi kusimama katika upande wa ukweli, na huwezi kutenda hata ukweli ulio wazi. Wanadamu kama hao hawawezi kuokolewa na ni wale ambao hawajashindwa. Kama kuingia kwako hakuna kina au malengo, kukua kwako kutakujia polepole. Kama kuingia kwako hakuna uhalisi hata kidogo, basi kufuatilia kwako kutakuwa bure. Kama hujui kiini cha ukweli, hutabadilishwa. Ukuaji katika maisha ya mwanadamu na mabadiliko katika tabia zake hupatikana kwa kuingia ndani ya ukweli na, zaidi ya hili, kwa kuingia katika uzoefu wa kina. Ukiwa na uzoefu wa kina katika wakati wa kuingia kwako, na ukiwa na ufahamu halisi kuhusu kuingia, tabia yako itabadilika haraka. Hata kama kwa sasa hujapata nuru sana katika vitendo, unafaa angalau upate nuru ya maono ya kazi. La sivyo utashindwa kuingia, na hutaweza kufanya hivyo isipokuwa uufahamu ukweli. Ni baada ya kuangaziwa nuru na Roho Mtakatifu katika uzoefu wako ndipo utakapopata ufahamu wa kina kuhusu ukweli na uingie kwa kina. Ni sharti uifahamu kazi ya Mungu.

Baada ya uumbaji wa mwanadamu hapo mwanzoni, Waisraeli ndio waliokuwa kielelezo cha kazi, na Israeli nzima ilikuwa ngome ya kazi ya Yehova duniani. Kazi ya Yehova ilikuwa imwongoze mwanadamu moja kwa moja na kumchunga kwa kuweka wazi sheria ili kwamba mwanadamu aweze kuishi maisha ya kawaida na kumwabudu Yehova kwa njia ya kawaida duniani. Katika Enzi ya Sheria Mungu alikuwa Asiyeonekana wala kuguswa na mwanadamu. Alikuwa tu Anawaongoza wanadamu waliokuwa mwanzo wamepotoshwa na Shetani, na Alikuwepo kuwaagiza na kuwaongoza wanadamu, kwa hivyo maneno yote Aliyoyanena yalikuwa ya kisheria, amri na maarifa ya kawaida ya kuishi maisha kama mwanadamu, na wala sio kuhusu ukweli unaomruzuku mwanadamu. Waisraeli chini ya uongozi Wake hawakuwa wale

waliopotoshwa zaidi na Shetani. Kazi Yake ya sheria ilikuwa tu hatua ya kwanza kabisa katika kazi ya ukombozi, mwanzo hasa wa kazi ya wokovu, na haikuwa inahusiana kamwe na mabadiliko katika tabia za kimaisha za mwanadamu. Kwa hivyo, mwanzoni mwa kazi ya ukombozi hapakuwa na haja Kwake kuwa katika mwili kwa ajili ya kazi Yake katika Israeli. Ndiyo maana Alihitaji kiungo, yaani, chombo ambacho kwacho Angemfikia mwanadamu. Kwa hivyo kukazuka miongoni mwa viumbe waliozungumza na kufanya kazi kwa niaba ya Yehova, na hivi ndivyo wana wa wanadamu na manabii walikuja kufanya kazi miongoni mwa wanadamu. Wana wa Adamu walifanya kazi miongoni mwa wanadamu kwa niaba ya Yehova. Ili waitwe na Yeye inamaanisha kuwa hao watu walipanga sheria kwa niaba ya Yehova na walikuwa miongoni mwa watu wa Israeli; na watu kama hao walikuwa makasisi walioangaliwa na kulindwa na Yehova, na Roho wa Yehova alifanya kazi ndani yao; walikuwa viongozi miongoni mwa wanadamu na wahudumu wa Yehova wa moja kwa moja. Manabii kwa upande mwingine ndio waliokuwa na jukumu la kunena na mataifa na makabila yote kwa niaba ya Yehova. Ndio vilevile waliotoa unabii kuhusu kazi ya Yehova. Wawe wanadamu au manabii, wote waliinuliwa na Roho wa Yehova Mwenyewe na walikuwa na kazi ya Yehova ndani yao. Miongoni mwa wanadamu, walikuwa ndio wale waliomwakilisha Yehova moja kwa moja; walifanya kazi tu kwa kuwa waliinuliwa na Yehova wala si kwa kuwa walikuwa miili ambamo Roho mtakatifu Mwenyewe alikuwa kapata mwili. Kwa hivyo, ingawa wao walifanya kazi na kuongea kwa niaba ya Mungu, hao wana wa mwanadamu na manabii wa Enzi ya Sheria hawakuwa mwili wa Mungu mwenye mwili. Hii ilikuwa kinyume hasa katika Enzi ya Neema na hatua ya mwisho, kwani kazi ya ukombozi na hukumu ya mwanadamu vilifanywa na Mungu katika mwili Mwenyewe, na hapakuwa na haja ya kukuza manabii na wanadamu kufanya kazi kwa niaba Yake. Machoni pa mwanadamu, hamna tofauti kubwa kati ya kiini na mbinu za kazi zao. Ni kwa sababu hii ndiyo mwanadamu anachanganya kati ya kazi ya Mungu mwenye mwili na ile ya manabii na wanadamu. Kimsingi, umbo la Mungu mwenye mwili lilikuwa sawa na lile la manabii na wanadamu. Mungu mwenye mwili alikuwa wa kawaida na halisi zaidi kuliko manabii. Kwa hivyo mwanadamu anashindwa kabisa kuwatofautisha. Mwanadamu huangazia maumbile peke yake bila kugundua kuwa japo wote hufanya kazi na kuongea, kuna tofauti kubwa kati yao. Kwa sababu uwezo wa mwanadamu wa kung'amua ni duni, mwanadamu anashindwa kung'amua mambo ya kimsingi na hata zaidi hawezi kubainisha kitu changamano. Maneno na kazi za manabii na za wale waliotumiwa na Roho Mtakatifu zote zilikuwa zinafanya wajibu wa mwanadamu, kutekeleza jukumu lake kama kiumbe na kufanya ambacho mwanadamu anapaswa kufanya. Hata hivyo, maneno na kazi za Mungu mwenye mwili ilikuwa ni kuendeleza huduma Yake. Ingawa umbo Lake lilikuwa lile la kiumbe, kazi Yake haikuwa kutimiza majukumu Yake bali Huduma Yake. Dhana “wajibu” inarejelea viumbe ilhali “huduma” inarejelea mwili wa Mungu mwenye mwili. Kuna tofauti kubwa kati ya haya mawili,

na haya mawili hayabadilishani nafasi. Kazi ya mwanadamu ni kufanya wajibu wake, ilhali kazi ya Mungu ni kusimamia, na kuendeleza huduma Yake. Kwa hivyo, ingawa mitume wengi walitumiwa na Roho Mtakatifu na manabii wengi wakajazwa na Yeye, kazi zao na maneno yao yalikuwa tu kutimiza wajibu wao kama viumbe. Ingawa unabii wao ungeweza kuwa mkubwa kuliko maisha kama yanavyozungumziwa na Mungu mwenye mwili, na hata ubinadamu wao ulikuwa wa hali ya juu kuliko wa Mungu kuwa mwenye mwili, walikuwa bado wanafanya wajibu wao na wala si kutimiza huduma yao. Wajibu wa mwanadamu unarejelea majukumu yake, na ni kitu kinachoweza kupatwa kwa mwanadamu. Hata hivyo, huduma ifanywayo na Mungu mwenye mwili inahusiana na usimamizi Wake, na haiwezi kufanikishwa na mwanadamu. Hata kama Mungu mwenye mwili hunena, kufanya kazi, au kutenda miujiza, Anafanya kazi kubwa katika usimamizi Wake, kazi ambayo haiwezi kufanywa na mwanadamu kwa niaba Yake. Kazi ya mwanadamu ni kufanya tu wajibu wake kama kiumbe katika hatua fulani ya usimamizi wa Mungu. Bila usimamizi kama huo, yaani, ikiwa huduma ya Mungu mwenye mwili itapotea, pia wajibu wa viumbe utapotea. Kazi ya Mungu kuendeleza huduma Yake ni kumsimamia mwanadamu, ilhali mwanadamu afanyapo wajibu wake ni kutimiza wajibu wake ili kuafikia masharti ya Muumba na haiwezi kwa vyovyote vile kuchukuliwa kwamba ameendeleza huduma ya mtu yeyote. Kwa kiini asili cha Mungu, yaani, Roho, kazi ya Mungu ni usimamizi wake, bali kwa Mungu mwenye mwili akiwa na umbile la nje la kiumbe, kazi yake ni kuendeleza huduma Yake. Kazi yoyote Aifanyayo ni ya kuendeleza huduma Yake, na mwanadamu anaweza tu kufanya awezalo ndani ya upeo Wake wa usimamizi na chini ya uongozi Wake.

Mwanadamu kufanya wajibu wake ni, kwa uhakika, kutimiza yote yaliyo ya asili yake, yaani, yale yawezekanayo kwa mwanadamu. Hapo ndipo wajibu wake hutimizika. Dosari za mwanadamu wakati wa huduma ya mwanadamu hupunguzwa taratibu kupitia kwa uzoefu uongezekao na mchakato wa uzoefu wake wa hukumu; hayazuii au kuathiri wajibu wa mwanadamu. Wanaoacha kutoa huduma au kuzalisha na kurudi nyuma kwa kuogopa makosa yanayoweza kuwepo katika huduma ndio waoga zaidi miongoni mwa wanadamu wote. Ikiwa mwanadamu haonyeshi anachopaswa kuonyesha wakati wa kutoa huduma au kutimiza kile kilicho katika uwezo wake kiasili, na badala yake huzembea na kufanya tu bila ari yoyote, atakuwa amepoteza majukumu yake ambayo kiumbe anapaswa kuwa nayo. Mwanadamu kama huyu anachukuliwa kuwa mtu hafifu na duni apotezaye nafasi; itakuaje kwamba mtu kama huyu aitwe kiumbe? Je, hao si ni vyombo vya upotovu ving'aavyo kwa nje ila vimeoza kwa ndani? Ikiwa mwanadamu atajiita Mungu lakini hawezi kuonyesha uungu na kufanya kazi ya Mungu Mwenyewe, au amwakilishe Mungu, bila shaka si Mungu kwani hana sifa za Mungu, na kile ambacho Mungu Anaweza kukitimiza hakimo ndani yake. Mwanadamu akipoteza kile ambacho

chaweza kutimizwa kiasili, hawezi kamwe kuitwa mwanadamu, na hafai kusimama kama kiumbe aliyeumbwa au kuja mbele za Mungu na kumtolea huduma. Aidha, hafai kupokea neema ya Mungu au kutunzwa, kulindwa na kukamilishwa na Mungu. Wengi waliopoteza imani ya Mungu hatimaye hupoteza neema Yake. Si kwamba wanachukia makosa yao tu bali pia hueneza wazo kuwa njia ya Mungu si sahihi. Na wale waasi hupinga hata uwepo wa Mungu; itakuwaje watu wenye uasi kama huo waendeleo kupata neema ya Mungu? Wanadamu walioshindwa kutekeleza wajibu wao wameasi sana dhidi ya Mungu na wanawiwa mengi na Yeye, lakini wanageuka na kumkong'ota Mungu kwamba ni mkosaji. Je, mwanadamu kama huyo anastahili vipi kufanywa mkamilifu? Je, si huyu ni mmoja wa wale watakoondolewa na kuadhibiwa? Mwanadamu asiyefanya wajibu wake mbele za Mungu tayari ana hatia ya makosa mazito sana ambayo hata kifo si adhabu stahili, ila bado mwanadamu ana ufidhuli wa kubishana na Mungu na kujilinganisha na Yeye. Pana faida gani kumkamilisha mwanadamu sampuli hiyo? Kama mwanadamu ameshindwa kutekeleza wajibu wake, anafaa kujihisi mwenye hatia na mdeni; anapaswa kuudharau udhaifu wake na kukosa umuhimu, uasi na uharibifu wake, na zaidi ya hayo, anafaa kujitolea maisha na damu sadaka kwa ajili ya Mungu. Hapo tu ndipo atakapokuwa kiumbe ampendaye Mungu kwa kweli, na ni mwanadamu kama huyu tu anayestahili baraka na ahadi za Mungu, na kukamilishwa na Yeye. Na wengi wenu je? Mnamtendeaje Mungu aishiye miongoni mwenu? Mmefanyaje wajibu wenu mbele Zake? Je, mmefanya yote mliyoitwa kufanya, hata kwa gharama ya maisha yenu? Mmetoa sadaka gani? Je, hamjapokea mengi kutoka Kwangu? Mnaweza kuonyesha tofauti? Mna uaminifu kiasi gani Kwangu? Mmenitolea huduma vipi? Na kuhusu yote Niliyowapa na kuwafanyia je? Je, mmeyazingatia yote? Je, mmeyahukumumu na kuyalinganisha haya yote kwa dhamiri yoyote ndogo mliyo nayo? Maneno na matendo yenu yanawezaje kuwa ya kustahili? Je, yawezekana hizo sadaka zenu kidogo zinalingana na yote Niliyowapa? Sina chaguo jingine na Nimejitolea kwenu kwa moyo wote, na bado mna nia zenye uovu kunihusu na hamnipendi kwa dhati. Huo ndio upeo wa wajibu wenu, jukumu lenu la pekee. Au sivyo? Hamjui kwamba hamjatimiza wajibu wa kiumbe aliyeumbwa hata kidogo? Mnawezaje kuchukuliwa kama kiumbe aliyeumbwa? Je, hamjui wazi mnachopaswa kuonyesha nakuishi kwa kudhihirisha katika maisha yenu? Mmeshindwa kutimiza wajibu wenu, ila mnataka mpate huruma na neema tele za Mungu. Neema hiyo haijaandaliwa kwa wasio na thamani na wa hali duni kama nyinyi, bali kwa wale ambao hawaombi kitu ila wanatoa kwa moyo wa dhati. Wanadamu kama nyinyi, watu duni, hawastahili kufurahikia neema ya mbinguni. Ni ugumu tu wa maisha na adhabu isiyokoma vitayaandama maisha yenu! Ikiwa hamwezi kuwa waaminifu Kwangu, majaaliwa yenu yatakuwa matatizo. Ikiwa hamwezi kuyawajibikia maneno Yangu na kazi Yangu, kundi lenu litakuwa la kuadhibiwa. Kamwe hamtapata neema, na hamtakuwa na baraka na maisha ya kupendeza katika ufalme. Hii ndiyo hatima na matokeo mnayostahili kupata kwa kujitakia! Hao watu wapumbavu na mafidhuli

hawajafanya kila wawezalo wala kutimiza wajibu wao tu, bali wameinyoosha mikono yao wakitaka neema, kana kwamba wanastahili wanachoitisha. Na wakishindwa kupata wanachokiomba, wanakuwa wakosa imani zaidi. Watu kama hao wanawezaje kuchukuliwa kuwa wenye mantiki? Ninyi ni sampuli mbaya isiyokuwa na urazini, isiyoweza kabisa kutimiza wajibu mnaotakiwa kutimiza wakati wa kazi ya usimamizi. Thamani yenu tayari imeshuka pakubwa. Kushindwa kwenu kunilipa kwa kuwaonea imani tayari ni tendo la uasi mkuu litoshalo kuwahukumu na kuthibitisha uoga, uovu, uzembe na uduni wenu. Mnawezaje kuendelea kustahili kunyoosha mikono yenu? Hamwezi kuwa hata wa msaada kidogo kwa kazi Yangu, hamwezi kuahidi imani yenu, na hamwezi kunitolea ushuhuda. Tayari haya ni makosa na kushindwa kwenu, na bado mnanivamia, mnanisemea uongo na kulalama kuwa Mimi si mwenye haki. Je, huu ndio uaminifu wenu? Huu ndio upendo wenu? Ni kazi gani nyingine mnayoweza kufanya zaidi ya hii? Mmechangia vipi katika kazi yote ambayo imeishafanywa? Mmegharamia kiasi gani? Ni huruma kubwa tayari kwamba bado Sijawawekea lawama, na bado mnanipa visingizio na kulalama faraghani kunihusu. Kweli mna hata chembe ndogo ya ubinadamu? Ingawa wajibu wa mwanadamu umetiwa doa na fikira za mwanadamu na mitazamo yake, ni sharti ufanye wajibu wako na kuwa mwaminifu kwa imani yako. Uchafu katika kazi ya mwanadamu ni suala la ubora wa tabia yake, ilhali, ikiwa mwanadamu hafanyi wajibu wake, unajisi huu unaonyesha uasi wake. Hakuna uhusiano kati ya wajibu wa mwanadamu na endapo amebarikiwa au amelaaniwa. Wajibu ni kile ambacho mwanadamu anapaswa kutimiza; ni wajibu wake na haategemei fidia, masharti, au sababu. Hapo tu ndipo huko kutakuwa kufanya wajibu wake. Mwanadamu aliyebarikiwa hufurahia wema baada ya kufanywa mkamilifu baada ya hukumu. Mwanadamu aliyelaaniwa hupokea adhabu tabia yake isipobadilika hata baada ya kutiwa adabu na kuhukumiwa, yaani, hajakamilishwa. Kama kiumbe, mwanadamu anapaswa kutimiza wajibu wake, afanye anachopaswa kufanya, na afanye anachoweza kufanya, bila kujali kama atabarikiwa au kulaaniwa. Hili ndilo sharti la msingi kwa mwanadamu, kama anayemtafuta Mungu. Usifanye wajibu wako ili ubarikiwe tu, na usikatae kutenda kwa kuogopa kupata laana. Acha Niwaambie hiki kitu kimoja: Ikiwa mwanadamu anaweza kufanya wajibu wake, inamaanisha kuwa anafanya anachopaswa kufanya. Ikiwa mwanadamu hawezi kufanya wajibu wake, inaonyesha uasi wake. Kila mara ni katika harakati ya kufanya wajibu wake ndipo mwanadamu polepole anabadilishwa, na ni katika harakati hii ndipo anapoonyesha utiifu wake. Kwa hivyo, kadiri uwezavyo kufanya wajibu wako, ndivyo ukweli utakaopokea unavyoongezeka, na vivyo hivyo mwonekano wako utakuwa halisi zaidi. Wale ambao hufanya tu mambo bila ari yoyote katika kufanya wajibu wao na hawautafuti ukweli mwishowe wataondolewa, kwani watu kama hao hawafanyi wajibu wao katika utendaji wa ukweli, na hawatendi ukweli katika kutekeleza wajibu wao. Watu kama hao ni wale wanaobaki bila kubadilika na watalaaniwa. Misemo yao haijajaa najisi tu, ila wakitamkacho si kingine bali ni

uovu.

Katika Enzi ya Neema, Yesu pia Alinena mengi na kufanya kazi nyingi. Alikuwa je tofauti na Isaya? Alikuwa je tofauti na Danieli? Je, Alikuwa nabii? Ni kwa nini inasemekana kwamba Yeye ni Kristo? Kuna tofauti gani baina yao? Wote walikuwa wanadamu walionena maneno, na maneno yao yalionekana sawa kwa wanadamu. Wote walinena na kufanya kazi. Manabii wa Agano la Kale walitoa unabii, na vivyo hivyo, pia na Yesu. Ni kwa nini iwe hivi? Tofauti hapa inapatikana katika aina ya kazi zao. Ili kutambua suala hili, huwezi kuangazia asili ya mwili na hufai kuangazia upurukushani wa maneno ya mtu. Daima ni sharti kwanza uangazie kazi yake na athari ambayo kazi yake inafanikisha ndani ya mwanadamu. Unabii uliotolewa na manabii wakati ule, haukuyaruzuku maisha ya mwanadamu, na ujumbe uliopokelewa na watu kama Isaya na Danieli ulikuwa tu unabii na si njia ya uzima. Ingekuwa si kuonekana moja kwa moja kwa Yehova, hakuna ambaye angefanya hiyo kazi, ambayo haiwezekani kwa wanadamu. Yesu pia Alisema mengi, lakini maneno yake yalikuwa njia ya uzima ambayo kwayo mwanadamu angepata njia ya kutenda. Hii ni kusema kuwa, kwanza, Angeukimu uzima wa mwanadamu, kwa kuwa Yesu ni uzima; pili, Angeweza kuugeuza upotovu wa mwanadamu; tatu, kazi Yake ingeweza kuifuata ile ya Yehova ili kuendeleza enzi; nne, Angeweza kutambua mahitaji ya mwanadamu kwa ndani na kufahamu anachokosa mwanadamu; tano, Angeweza kuanzisha enzi mpya na kutamatisha enzi ya zamani. Ndiyo maana Anaitwa Mungu na Kristo; Yeye si tofauti na Isaya tu; bali pia na manabii wengine wote. Chukua Isaya kama ulinganisho wa kazi za manabii. Kwanza, asingeweza kuukimu uzima wa mwanadamu; pili, asingeweza kuanzisha enzi mpya. Alikuwa akifanya kazi chini ya uongozi wa Yehova wala si kuanzisha enzi mpya. Tatu, alichokizungumza yeye mwenyewe kilikuwa nje ya ufahamu wake. Alikuwa akipata ufunuo moja kwa moja kutoka kwa Roho wa Mungu, na wengine wasingeelewa hata baada ya kuusikiliza ufunuo huo. Haya machache yanatosha kuthibitisha kuwa kazi yake haikuwa zaidi ya unabii, si zaidi ya kazi iliyofanywa kwa niaba ya Yehova. Hata hivyo, asingeweza kumwakilisha Yehova kikamilifu. Alikuwa mtumishi wa Yehova, chombo katika kazi ya Yehova. Aidha alikuwa anafanya kazi katika Enzi ya Sheria tu na katika mawanda ya kazi ya Yehova; hakufanya kazi nje ya Enzi ya Sheria. Kinyume na haya, kazi ya Yesu ilikuwa tofauti. Alivuka mipaka ya kazi ya Yehova; Alifanya kazi kama Mungu mwenye mwili na kupitia mateso ili amkomboe mwanadamu. Hiyo ni kusema kuwa Alifanya kazi mpya nje ya ile iliyofanywa na Yehova. Huku kulikuwa kukaribisha kwa enzi mpya. Jambo jingine ni kuwa Aliweza kuyazungumzia mambo ambayo mwanadamu asingeweza kupata. Kazi Yake ilikuwa kazi ndani ya usimamizi wa Mungu na ilijumuisha wanadamu wote. Hakufanya kazi miongoni mwa watu wachache tu, na wala kazi yake haikuwa kuwaongoza watu wachache tu. Kuhusu jinsi Mungu alivyopata mwili kuwa mwanadamu, jinsi Roho alivyotoa ufunuo wakati ule, na jinsi Roho

alivyomshukia mwanadamu kufanya kazi, haya ni mambo ambayo mwanadamu hawezi kuona au kugusa. Haiwezekani kabisa ukweli huu kuwa thibitisho kuwa Yeye ni Mungu mwenye mwili. Kwa sababu hii, tofauti inaweza kupatikana tu kwenye maneno na kazi ya Mungu ambayo ni mambo dhahiri kwa mwanadamu. Hili tu ndilo halisi. Hii ni kwa sababu masuala ya Roho hayaonekani kwako na yanafahamika wazi na Mungu Mwenyewe peke Yake, wala hata mwili wa Mungu haufahamu yote; unaweza kuthibitisha tu kama Yeye ni Mungu^[a] kutokana na kazi Aliyofanya tu. Kutokana na kazi Yake, inaweza kuonekana kuwa, kwanza, Anaweza kufungua enzi mpya; pili, Yeye ana uwezo wa kuyaruzuku maisha ya mwanadamu na kumwonyesha mwanadamu njia ya kufuata. Hii inatosha kuthibitisha kuwa Yeye ni Mungu Mwenyewe. Angalau kazi Aifanyayo yaweza kumwakilisha kikamilifu Roho Mtakatifu wa Mungu na kutokana na kazi hiyo inaonekana kuwa Roho wa Mungu yupo ndani Yake. Kwa kuwa kazi iliyoifanywa na Mungu mwenye mwili ilikuwa kuanzisha enzi mpya, kuongoza kazi mpya, na kuanzisha na kufungua mazingira mapya, haya mambo machache tu yanatosha kuthibitisha kuwa Yeye ni Mungu Mwenyewe. Hili kwa hivyo linamtofautisha na Isaya, Danieli, na manabii wengine wakuu. Isaya, Danieli na wengine wote walikuwa ni watu walioelimika na kustaarabika vilivyo; walikuwa watu wa kipekee chini ya uongozi wa Yehova. Mwili wa Mungu mwenye mwili pia ulikuwa na maarifa na haukupungukiwa na akili ila ubinadamu Wake ulikuwa wa kawaida. Alikuwa mwanadamu wa kawaida na jicho la mwanadamu lisingeweza kubaini ubinadamu wowote wa pekee kumhusu au kugundua kitu chochote katika ubinadamu Wake tofauti na wa wale wengine. Kamwe hakuwa kabisa wa kimiujiza au wa kipekee na hakuwa na elimu ya juu, ujuzi au nadharia kupita kiasi. Maisha Aliyoyazungumzia na njia Aliyoenenda hakuipata kinadharia, kielimu, kitajriba au kupitia malezi ya kifamilia. Badala yake, ilikuwa kazi ya moja kwa moja ya Roho, ambayo ni kazi ya mwili. Ni kwa kuwa mwanadamu ana mawazo makuu kumhusu Mungu, na hasa kwa kuwa fikira hizi hutungwa kutokana na vipengele vingi visivyo yakini na vya kimiujiza hivi kwamba, katika macho ya mwanadamu, Mungu wa kawaida mwenye udhaifu wa kibinadamu, ambaye hawezi kutenda miujiza, kwa hakika si Mungu. Je, si hizi ni fikra potovu za mwanadamu? Mwili wa Mungu mwenye mwili usingekuwa wa kawaida, basi ingesemekanaje kwamba Alipata mwili? Kupata mwili ni kuwa mtu wa kawaida; iwapo angekuwa wa kupita uwezo wa binadamu, basi Asingeweza kuwa wa kimwili. Kuthibitisha kuwa Yeye ni wa kimwili, Mungu mwenye mwili alihitaji kuwa na mwili wa kawaida. Hili lilikusudiwa tu kutimiza umuhimu wa kupata mwili. Hata hivyo, mambo hayakuwa hivyo kwa manabii na wanadamu. Walikuwa wanadamu waliopewa vipawa na kutumiwa na Roho Mtakatifu; machoni mwa mwanadamu, ubinadamu wao ulikuwa wa hali ya juu, walitenda matendo mengi yaliyovuka mipaka ya ubinadamu wa kawaida. Kwa sababu hii mwanadamu aliwachukulia kama Mungu. Sasa ni sharti nyote mlione hili kwa uwazi zaidi, kwani limekuwa jambo ambalo liliwakanganya sana wanadamu wote katika enzi zilizopita. Aidha, kuwa mwili

ndicho cha ajabu zaidi kwa vitu vyote, na Mungu mwenye mwili ni vigumu zaidi kukubaliwa na mwanadamu. Ninachokisema kinasaidia katika kutimiza majukumu yenu na kuelewa kwenu kwa fumbo la kupata mwili. Haya yote yanahusiana na usimamizi wa Mungu, kwa maono. Ufahamu wenu wa hili jambo utakuwa wa faida zaidi kwa kupata ufahamu wa maono, yaani kazi ya usimamizi. Kwa njia hii, mtafahamu zaidi pia wajibu ambao wanadamu mbalimbali wanafaa kutekeleza. Ingawa maneno haya hayawaonyeshi njia moja kwa moja, bado ni msaada mkubwa kwa kuingia kwenu, kwa kuwa maisha yenu ya sasa yamepungukiwa sana na maono na hili litakuwa kikwazo kikubwa kinachozuia kuingia kwenu. Kama hamjaweza kuyafahamu masuala haya, basi hakutakuwa na motisha ya kuchochea kuingia kwenu. Na kufuatilia kama huku kunawezaje kuwawezesha kutimiza wajibu wenu vyema zaidi?

Tanbihi:

a. Maandiko asili hayana kauli “kama Yeye ni Mungu.”

Mungu Ndiye Bwana wa Viumbe Vyote

Hatua moja ya kazi ya enzi mbili za awali ilifanyika Israeli; nyingine ilifanyika Yudea. Kuzungumza kwa jumla, hakuna hatua ya kazi hii iliyoondoka Israeli; zilikuwa ni hatua za kazi zilizofanywa miongoni mwa wateule wa mwanzo. Hivyo, kwa mtazamo wa Waisraeli, Yehova Mungu ni Mungu wa Waisraeli pekee. Kwa sababu ya kazi ya Yesu huko Yudea, na kwa sababu ya kukamilisha Kwake kazi ya kusulubiwa, kwa mtazamo wa Wayahudi, Yesu ni Mkombozi wa watu wa Kiyahudi. Yeye ni Mfalme wa Wayahudi pekee, sio wa watu wengine wowote; Yeye si Bwana anayewakomboa Waingereza, wala Bwana anayewakomboa Wamarekani, lakini Yeye ni Bwana anayewakomboa Waisraeli, na katika Israeli ni Wayahudi ndio Anaowakomboa. Kwa kweli, Mungu ni Bwana wa mambo yote. Yeye ndiye Mungu wa viumbe vyote. Yeye si Mungu wa Waisraeli pekee, na Yeye si Mungu wa Wayahudi pekee; Yeye ni Mungu wa viumbe vyote. Hatua mbili za awali za kazi Yake zilifanyika Israeli, na kwa njia hii, dhana zingine zimejitokeza ndani ya watu. Watu wanafikiri kuwa Yehova alikuwa akifanya kazi Israeli na Yesu Mwenyewe alitekeleza kazi Yake Yudea—zaidi ya hayo, ilikuwa kupitia kupata mwili ambapo Alikuwa akifanya kazi Yudea—na kwa vyovyote, kazi hii haikuenea zaidi ya Israeli. Hakuwa akifanya kazi na Wamisri; Hakuwa akifanya kazi na Wahindi; Alikuwa tu akifanya kazi na Waisraeli. Watu basi wanaunda dhana mbalimbali; aidha, wanapanga kazi ya Mungu ndani ya eneo fulani. Wanasema kwamba wakati Mungu anafanya kazi, ni lazima ifanywe miongoni mwa wateule na ndani ya Israeli; mbali na Waisraeli, Mungu hana mpokeaji mwingine wa kazi Yake, wala Hana eneo lingine la kazi Yake; ni wakali hasa katika “kumfundisha nidhamu” Mungu mwenye mwili, kutomruhusu kuenda zaidi ya eneo la Israeli. Je, hizi zote si dhana za binadamu? Mungu aliunda mbingu na dunia yote na vitu vyote, na kuumba viumbe vyote; Angewezaje kuzuia kazi Yake

ndani ya Israeli peke yake? Katika hali hiyo, kungekuwa na haja gani ya Yeye kuumba viumbe Vyake vyote? Aliiumba dunia nzima; Ametekeleza mpango Wake wa usimamizi wa miaka elfu sita sio tu ndani ya Israeli lakini pia na kila mtu ulimwenguni. Bila kujali kama anaishi Uchina, Amerika, Uingereza ama Urusi, kila mtu ni wa ukoo wa Adamu; wote wameumbwa na Mungu. Hakuna mtu hata mmoja anayeweza kuondoka katika mawanda ya viumbe wa Mungu, na hakuna mtu hata mmoja anayeweza kuepuka utambulisho wa “ukoo wa Adamu.” Wote ni viumbe wa Mungu, na wote ni wa ukoo wa Adamu; pia ni wazawa wapotovu wa Adamu na Hawa. Sio tu Waisraeli ambao ni viumbe wa Mungu, lakini ni watu wote; hata hivyo, wengine miongoni mwa viumbe wamelaaniwa, na wengine wamebarikiwa. Kuna mambo mengi ya kupendeza kuwahusu Waisraeli; Mungu awali alikuwa akifanya kazi nao kwa sababu walikuwa watu wapotovu kwa kiasi kidogo zaidi. Wachina ni dhaifu wakilinganishwa nao, na hawawezi hata kutumaini kulingana nao; hivyo, Mungu awali alifanya kazi miongoni mwa watu wa Israeli, na hatua ya pili ya kazi Yake ilifanywa tu Yudea. Kwa sababu hii, watu huunda dhana nyingi na kanuni nyingi. Kwa kweli, iwapo Angetenda kulingana na dhana za binadamu, Mungu angekuwa tu Mungu wa Waisraeli; kwa njia hii Asingeweza kupanua kazi Yake katika mataifa yasiyo ya Kiyahudi, kwa sababu Angekuwa tu Mungu wa Waisraeli badala ya Mungu wa viumbe vyote. Unabii ulisema kuwa jina la Yehova lingekuwa kubwa katika mataifa yasiyo ya Kiyahudi na kuwa jina la Yehova lingenezwa kwa mataifa yasiyo ya Kiyahudi—mbona ulisema hivi? Iwapo Mungu angekuwa Mungu wa Waisraeli tu, basi Angefanya kazi tu Israeli. Zaidi ya hayo, Asingepanua kazi hii, na Asingefanya huu unabii. Kwa sababu Alifanya huu unabii, Angehitaji kuipanua kazi Yake hadi mataifa yasiyo ya Kiyahudi na hadi kila taifa na mahali. Kwa sababu Alisema hili, basi Angefanya hivyo. Huu ndio mpango Wake, kwani Yeye ndiye Bwana aliyeumba mbingu na dunia na vitu vyote, na Mungu wa viumbe vyote. Bila kujali iwapo Anafanya kazi na Waisraeli ama katika Yudea nzima, kazi Anayoifanya ni kazi ya ulimwengu mzima na kazi ya binadamu wote. Kazi Anayoifanya leo katika taifa la joka kubwa jekundu—katika taifa lisilo la Kiyahudi—bado ni kazi ya binadamu wote. Israeli inaweza kuwa kituo cha kazi Yake duniani; vivyo hivyo, Uchina pia inaweza kuwa kituo cha kazi Yake miongoni mwa mataifa yasiyo ya Kiyahudi. Je, sasa Hajatimiza unabii kwamba “jina la Yehova litakuwa kubwa katika mataifa yasiyo ya Kiyahudi”? Hatua ya kwanza ya kazi Yake miongoni mwa mataifa yasiyo ya Kiyahudi inahusu kazi hii Anayoifanya katika taifa la joka kuu jekundu. Kwa Mungu mwenye mwili kufanya kazi katika nchi hii na kufanya kazi miongoni mwa hawa watu waliolaaniwa hasa inaenda kinyume na dhana za binadamu; hawa watu ni wa chini zaidi na wasio na thamani yoyote. Hawa wote ni watu ambao Yehova alikuwa amewaacha mwanzoni. Watu wanaweza kuachwa na watu wengine, lakini wakiachwa na Mungu, hawa watu hawatakuwa na hadhi, na watakuwa na thamani ya kiwango cha chini zaidi. Kama sehemu ya viumbe, kumilikiwa na Shetani ama kuachwa na watu wengine yote mawili ni mambo

machungu, lakini sehemu ya viumbe ikiachwa na Bwana wa viumbe, hii inaashiria kwamba hadhi yake iko katika kiwango cha chini kabisa. Wazawa wa Moabu walilaaniwa, na walizaliwa ndani ya nchi hii isiyo na maendeleo; bila shaka, wazawa wa Moabu ni watu walio na hadhi ya chini zaidi chini ya ushawishi wa giza. Kwa sababu hawa watu walimiliki hadhi ya chini zaidi zamani, kazi inayofanywa miongoni mwao inaweza kabisa kuzivunja dhana za binadamu, na pia ni kazi yenye faida kubwa zaidi kwa mpango Wake mzima wa usimamizi wa miaka elfu sita. Ili Afanye kazi miongoni mwa watu hawa ni kitendo kinachoweza zaidi kuzivunja dhana za binadamu; Akiwa na hili Anazindua enzi; na hili Anavunja dhana zote za binadamu; Akiwa na hili Anatamatisha kazi ya Enzi nzima ya Neema. Kazi Yake ya awali ilifanywa Yudea, ndani ya eneo la Israeli; katika mataifa yasiyo ya Kiyahudi Hakufanya kazi yoyote ya uzinduzi wa enzi hata kidogo. Hatua ya mwisho ya kazi Yake haifanywi tu miongoni mwa watu wa mataifa yasiyo ya Kiyahudi; hata zaidi ya hayo, inafanywa miongoni mwa watu waliolaaniwa. Jambo hili moja ndio ushahidi unaoweza zaidi kumwaibisha Shetani; hivyo, Mungu “anakuwa” Mungu wa viumbe vyote ulimwenguni na kuwa Bwana wa vitu vyote, Anayeabudiwa na kila kiumbe mwenye uhai.

Kwa sasa bado kuna watu wengine wasioelewa ni aina gani ya kazi mpya ambayo Mungu amezindua. Mungu amefanya mwanzo mpya katika mataifa yasiyo ya Kiyahudi na Ameanza enzi nyingine na kuzindua kazi nyingine, na Anafanya kazi miongoni mwa ukoo wa Moabu. Je, hii si kazi Yake mpya kabisa? Hakuna yeyote katika enzi zote aliyeipitia kazi hii, wala hakuna aliyeisikia, sembuse kuithamini. Hekima ya Mungu, ajabu ya Mungu, kutoeleweka kwa Mungu, ukubwa wa Mungu, utakatifu wa Mungu vinategemea hatua hii ya kazi katika siku za mwisho, ili kuibuka wazi. Je, hii si kazi mpya inayovunja dhana za binadamu? Bado kuna wale wanaofikiria hivi: “Kwa sababu Mungu alimlaani Moabu na kusema kuwa Angewaacha wazawa wa Moabu, Angeweza kuwaokoaje sasa?” Hao ni wale watu kutoka mataifa yasiyo ya Kiyahudi waliolaaniwa na kulazimishwa nje ya Israeli; Waisraeli waliwaita “mbwa wasio wa Kiyahudi.” Kwa mtazamo wa kila mtu, wao sio mbwa wasio wa Kiyahudi pekee, lakini mbaya hata zaidi, ni wana wa maangamizi; kwa maneno mengine, wao si wateule wa Mungu. Ingawa awali walikuwa wamezaliwa ndani ya eneo la Israeli, wao siyo sehemu ya watu wa Israeli; wao pia walifukuzwa kwenda kwa mataifa yasiyo ya Kiyahudi. Wao ndio watu wa chini zaidi. Ni kwa sababu hasa wao ni watu wa chini zaidi miongoni mwa binadamu ndio Mungu anatekeleza kazi Yake ya kuzindua enzi mpya miongoni mwao, kwani wao ni wawakilishi wa binadamu wapotovu. Kazi ya Mungu haikosi uchaguzi ama madhumuni, kazi Anayoifanya miongoni mwa watu hawa leo pia ni kazi inayofanywa miongoni mwa viumbe. Nuhu alikuwa sehemu ya viumbe, kama walivyo wazawa wake. Yeyote duniani aliye na mwili na damu ni sehemu ya viumbe. Kazi ya Mungu imeelekezwa kwa viumbe wote; haitekelezwi kulingana na kama mtu amelaaniwa baada

ya kuumbwa. Kazi Yake ya usimamizi imeelekezwa kwa viumbe wote, sio wale wateule wasiolaaniwa. Kwa sababu Mungu anataka kutekeleza kazi Yake miongoni mwa viumbe Vyake, kwa hakika Ataifanya hadi kukamilika kwa mafanikio; Atafanya kazi miongoni mwa hao watu walio na manufaa kwa kazi Yake. Kwa hivyo, Anavunja mikataba yote ya kufanya kazi miongoni mwa watu; Kwake, maneno “kulaaniwa,” “kuadibu” na “kubarikiwa” hayana maana! Wayahudi ni wazuri hasa, na wateule wa Israeli sio wabaya pia; ni watu wenye ubora mzuri wa tabia na ubinadamu mzuri. Awali Yehova alizindua kazi Yake miongoni mwao na Akafanya kazi Yake ya awali, lakini ingekuwa bila maana kama Angewatumia kama wapokeaji wa kazi Yake ya ushindi sasa. Ingawa wao pia ni sehemu ya viumbe na wana vipengele vingi vyema, ingekuwa bila maana kutekeleza hatua hii ya kazi miongoni mwao. Asingeweza kumshinda yeyote, wala Asingeweza kushawishi viumbe wote. Huu ndio umuhimu wa uhamisho wa kazi Yake kwa watu hawa wa taifa la joka kubwa jekundu. Maana ya ndani zaidi hapa ni ya uzinduzi Wake wa enzi, ya kuvunja Kwake kwa kanuni zote na dhana zote za mwanadamu na pia kwa kumaliza Kwake kazi ya Enzi nzima ya Neema. Kama kazi Yake ya sasa ingefanywa miongoni mwa Waisraeli, ikifika wakati ambao mpango Wake wa usimamizi wa miaka elfu sita kukamilika, kila mtu angeamini kuwa Mungu ni Mungu tu wa Waisraeli, kuwa Waisraeli tu ndio wateule wa Mungu, kuwa Waisraeli tu ndio wanaostahili kurithi baraka na ahadi za Mungu. Katika siku za mwisho, Mungu anapata mwili katika taifa lisilo la Kiyahudi la joka kubwa jekundu; Ametimiza kazi ya Mungu kama Mungu wa viumbe wote; Amekamilisha kazi Yake yote ya usimamizi, na Atamaliza sehemu kuu ya kazi Yake kwa taifa la joka kubwa jekundu. Kiini cha hatua hizi tatu za kazi ni wokovu wa mwanadamu—ambao ni, kufanya viumbe wote vimwabudu Bwana wa viumbe. Hivyo basi, kila hatua ya kazi hii ni muhimu sana; Mungu hatafanya chochote kisicho na maana ama thamani. Kwa upande mmoja, hatua hii ya kazi inajumuisha kuzindua enzi na kukamilisha enzi mbili za awali; kwa upande mwingine inajumuisha kuvunja dhana zote za mwanadamu na njia ya zamani ya imani ya mwanadamu na maarifa. Kazi ya enzi mbili za awali ilifanywa kulingana na dhana tofauti za binadamu; hatua hii, hata hivyo, inafuta kabisa dhana za binadamu, na hivyo kuwashinda binadamu kikamilifu. Kwa kutumia ushindi wa ukoo wa Moabu na kutumia kazi iliyotekelezwa miongoni mwa ukoo wa Moabu, Mungu atawashinda binadamu wote katika ulimwengu mzima. Huu ndio umuhimu wa kina zaidi wa hatua hii ya kazi Yake, na ndicho kipengele cha thamani ya hatua hii ya kazi Yake. Hata kama sasa unajua kuwa hadhi yako ni ya chini na kuwa una thamani ya chini, bado utahisi kwamba umekutana na jambo linalofurahisha sana: Umerithi baraka kubwa, ukapata ahadi kubwa, na unaweza kamilisha hii kazi kubwa ya Mungu, na unaweza kuuona uso wa kweli wa Mungu, kujua tabia Yake ya asili, na kufanya mapenzi ya Mungu. Hatua mbili za awali za kazi ya Mungu zilifanywa Israeli. Iwapo hatua hii ya kazi Yake katika siku za mwisho bado ingefanywa miongoni mwa Waisraeli, viumbe wote havingeamini kwamba Waisraeli tu ndio waliokuwa wateule, lakini pia mpango wa

usimamizi wa Mungu wote haungefikia athari iliyotaka. Wakati ambapo hatua hizi mbili za kazi Yake zilifanywa Israeli, hakuna kazi yoyote mpya iliyokuwa imefanywa na hakuna kazi yoyote ya Mungu ya kuzindua enzi ilikuwa imewahi kufanywa katika mataifa yasiyo ya Kiyahudi. Hatua hii ya kazi ya kuzindua enzi inafanywa kwanza katika mataifa yasiyo ya Kiyahudi, na zaidi ya hayo, inafanywa kwanza miongoni mwa ukoo wa Moabu; hii imezindua enzi mpya. Mungu amevunja maarifa yoyote yaliyo ndani ya dhana za binadamu na hajaruhusu yoyote yaendeleo kuwa hai. Katika kazi Yake ya kushinda Amevunja dhana za binadamu, hiyo njia ya zamani, ya maarifa ya binadamu, Anaruhusu watu waone kuwa kwa Mungu hakuna kanuni, kwamba hakuna kitu kizee kumhusu Mungu, kwamba kazi Anayoifanya ni ya uhuru kabisa, ni huru kabisa, kwamba Yeye yuko sahihi katika chochote Anachofanya. Ni lazima utii kikamilifu kazi yoyote Anayoifanya miongoni mwa viumbe. Kazi yoyote Anayoifanya ni ya maana na inafanywa kulingana na mtazamo Wake na maarifa Yake na sio kulingana na chaguo za watu na dhana za watu. Anafanya yale mambo yaliyo na manufaa kwa kazi Yake; kama kitu hakina manufaa kwa kazi Yake, Hata kifanya, hata kiwe kizuri vipi! Anafanya kazi na kuchagua mpokeaji na eneo la kazi Yake kulingana na maana na madhumuni ya kazi Yake. Hafuati kanuni za zamani, wala Hafuati fomula nzee; badala yake, Anapanga kazi Yake kulingana na umuhimu wa kazi; mwishowe, Anataka kufikia matokeo yake ya kweli na madhumuni yanayotarajiwa. Iwapo huelewi mambo haya sasa, kazi hii haitatimiza matokeo yoyote kwako.

Msimamo Wako Kuhusu Nyaraka Kumi na Tatu ni Upi?

Agano Jipya la Biblia lina nyaraka kumi na tatu za Paulo. Katika muda aliofanya kazi yake, Paulo aliandika barua hizi kumi na tatu kwa makanisa yaliyoamini katika Yesu Kristo. Yaani, Paulo aliinuliwa na akaandika barua hizi baada ya Yesu kupaa mbinguni. Barua zake ni ushuhuda wa kufufuka na kupaa mbinguni kwa Bwana Yesu baada ya kifo Chake, na pia zilieneza njia ya toba na kubeba msalaba. Bila shaka, ujumbe na ushuhuda huu wote ulinuiwa kuwafunza ndugu katika maeneo tofauti huko Yudea wakati huo, kwa sababu wakati huo, Paulo alikuwa mtumishi wa Bwana Yesu, na alikuwa ameinuliwa kumshuhudia Bwana Yesu. Katika kila kipindi cha kazi ya Roho Mtakatifu, watu mbalimbali huinuliwa kutekeleza kazi Zake tofauti, yaani kufanya kazi ya mitume ili kuendeleza kazi ambayo Mungu anakamilisha Mwenyewe. Ikiwa Roho Mtakatifu angeifanya moja kwa moja, na hakuna watu wangeinuliwa, basi ingekuwa vigumu sana kwa kazi hiyo kutekelezwa. Kwa hiyo, Paulo akawa yule ambaye aliangushwa akiwa njiani kuelekea Dameski, na ambaye baada ya hapo aliinuliwa kumshuhudia Bwana Yesu. Alikuwa mtume kando na wanafunzi kumi na wawili wa Yesu. Juu ya kueneza injili, pia alifanyia makanisa ya maeneo mbalimbali kazi ya uchungaji, ambayo ilihusisha kuwatunza ndugu wa makanisa hayo—yaani, kuwaongoza ndugu katika Bwana. Ushuhuda wa Paulo ulikuwa ili kujulisha kuhusu kufufuka na kupaa mbinguni kwa Bwana Yesu, na vilevile

kuwafunza watu kutubu, kukiri, na kuitembea njia ya msalaba. Alikuwa mmoja wa mashahidi wa Yesu Kristo wa wakati huo.

Nyaraka kumi na tatu za Paulo zilichaguliwa ili zitumike katika Biblia. Aliandika hizo nyaraka zote kumi na tatu kuzungumzia hali tofauti za watu katika mahala mbalimbali. Aliguswa na Roho Mtakatifu kuziandika, na akawafunza ndugu kila mahali kutoka kwa nafasi ya mtume (kutoka kwa mtazamo wa mtumishi wa Bwana Yesu). Kwa hiyo, barua za Paulo hazikutoka kwa unabii au kutoka moja kwa moja kwa maono, bali zilitoka kwa kazi aliyoifanya. Barua hizi si za ajabu, wala si ngumu kuelewa kama unabii. Zinaandikwa tu kama barua, na hazina unabii wala mafumbo; zina maneno ya kawaida ya maagizo tu. Hata ingawa maneno yake mengi huenda yakawa magumu kwa watu kuyaelewa ama magumu kufahamu, yalitoka tu katika ufafanuzi wa Paulo mwenyewe na katika nuru ya Roho Mtakatifu. Paulo alikuwa mtume tu; alikuwa mtumishi aliyetumiwa na Bwana Yesu, si nabii. Alipokuwa akitembea katika nchi mbalimbali, aliwaandikia ndugu wa kanisa barua, ama, alipokuwa akiugua, aliyaandikia barua makanisa ambayo alikuwa akiyafikiria hasa lakini hakuweza kuyazuru. Kwa sababu hiyo, barua zake ziliwekwa na watu na baadaye zikakusanywa, kuratibiwa, na kupangwa baada ya Injili Nne katika Biblia na vizazi vya baadaye. Bila shaka, walichagua na kukusanya barua zote bora ambazo alikuwa ameandika. Nyaraka hizi zilinufaisha maisha ya ndugu wa kanisa, na hasa zilikuwa mashuhuri katika wakati wake. Paulo alipoziandika, lengo lake halikuwa kuandika kazi ya kiroho ambayo ingewawezesha ndugu zake wapate njia ya kutenda ama wasifu wa kiroho wa kuelezea aliyoyapitia yeye mwenyewe; hakunua kuandika kitabu ili awe mwandishi. Alikuwa tu akiwaandikia ndugu zake wa kanisa la Bwana Yesu barua. Kutoka kwa nafasi yake kama mtumishi, Paulo aliwafunza ndugu zake, akiwaambia kuhusu mzigo wake, kuhusu mapenzi ya Bwana Yesu, na kuhusu kazi ambazo Alikuwa amewaaminia watu wa siku za baadaye. Hii ilikuwa kazi ambayo Paulo alitekeleza. Maneno yake yaliadilisha sana uzoefu wa ndugu wote wa baadaye. Ukweli aliowasilisha katika barua hizi nyingi ulikuwa kile ambacho watu katika Enzi ya Neema walipaswa kutenda, na ndiyo sababu barua hizi zilipangwa katika Agano Jipya na vizazi vya baadaye. Bila kujali matokeo ya Paulo yaliishia kuwa yapi, alikuwa mtu ambaye alitumiwa katika wakati wake, na ambaye aliwasaidia ndugu katika makanisa. Matokeo yake yaliamuliwa na asili yake, na vilevile yeye kuangushwa mwanzoni. Aliweza kuyazungumzia maneno hayo wakati huo kwa sababu alikuwa na kazi ya Roho Mtakatifu, na Paulo aliyabebea makanisa mzigo kwa sababu ya kazi hii. Kwa hiyo, aliweza kuwaruzuku ndugu zake. Hata hivyo, kwa sababu ya hali fulani za kipekee, Paulo hakuweza kuenda kwa makanisa hayo kufanya kazi yeye binafsi, kwa hiyo aliyaandikia barua kuwaonya ndugu zake katika Bwana. Mwanzoni, Paulo aliwatesa wanafunzi wa Bwana Yesu, lakini baada ya Yesu kupaa mbinguni—yaani, baada ya Paulo “kuona mwangaza”—alikoma kuwatesa wanafunzi wa Bwana Yesu, na

hakuwatesa tena wale watakatifu waliohubiri injili kwa ajili ya njia ya Bwana. Baada ya Paulo kumwona Yesu akimwonekana kama mwanga mkali, alikubali agizo la Bwana, na hivyo akawa mtu aliyetumiwa na Roho Mtakatifu kueneza injili.

Kazi ya Paulo wakati huo ilikuwa tu kuwasaidia na kuwaruzuku ndugu zake. Hakuwa kama watu wengine, waliotaka kufanikiwa katika kazi yao ama kubuni kazi za fasihi, kuchunguza namna nyingine za mbadala, ama kupata njia kando na Biblia za kuwaongoza watu hawa katika makanisa ili wote waweze kuingia upya. Paulo alikuwa mtu aliyetumiwa; katika kufanya mambo aliyoyafanya, alikuwa tu akitimiza wajibu wake. Ikiwa hangeyabebea makanisa mzigo, basi angechukuliwa kuwa yule aliyetelekeza wajibu wake. Ikiwa jambo la kukatiza lingetokea, ama tukio la usaliti lingefanyika katika kanisa ambalo lingewasababisha watu hapo wawe na hali isiyo ya kawaida, basi angechukuliwa kuwa hakutekeleza kazi yake vizuri. Mfanyakazi akilibeeba kanisa mzigo, na pia afanye kazi vyema kadiri ya uwezo wake, basi hili linathibitisha kwamba mtu huyu ni mfanyakazi anayestahili—anayestahili kutumika. Mtu asipohisi mzigo wowote kwa ajili ya kanisa, na asitimize matokeo yoyote katika kazi yake, na watu wengi anaowaongoza ni dhaifu au hata wanaanguka, basi mfanyakazi kama huyu hajatimiza wajibu wake. Paulo alikuwa vivyo hivyo, na ndiyo sababu ilimbidi ayatunze makanisa na kuwaandikia ndugu zake barua mara kwa mara. Aliweza kuyaruzuku makanisa na kuwatunza ndugu zake kwa namna hii; ni kwa njia hii pekee ndiyo makanisa yaliweza kupokea ruzuku na uchungaji kutoka kwake. Maneno ya barua alizoandika yalikuwa ya maana sana, lakini yaliandikiwa ndugu zake chini ya sharti la yeye kupokea nuru ya Roho Mtakatifu, na alitia uzoefu wake binafsi na mzigo aliohisi ndani ya maandishi yake. Paulo alikuwa tu mtu aliyetumiwa na Roho Mtakatifu, na maudhui yote ya barua zake yalichanganywa na uzoefu wake binafsi. Kazi aliyoifanya inawakilisha tu kazi ya mtume, siyo kazi iliyotekelezwa moja kwa moja na Roho Mtakatifu, na pia inatofautiana na kazi ya Kristo. Paulo alikuwa tu akitimiza wajibu wake, ambayo ndiyo sababu aliwaruzuku ndugu zake katika Bwana kwa mzigo wake na vilevile uzoefu na umaizi wake binafsi. Paulo alikuwa tu akitekeleza kazi ya agizo la Mungu kwa kutoa umaizi na ufahamu wake binafsi; bila shaka huu haukuwa mfano wa kazi iliyotekelezwa moja kwa moja na Mungu Mwenyewe. Kwa hiyo, kazi ya Paulo ilichanganywa na uzoefu wa binadamu na maoni ya binadamu na ufahamu wa kazi ya kanisa. Hata hivyo, ufahamu na maoni haya ya binadamu hayawezi kusemekana kuwa kazi ya roho mbaya ama kazi ya mwili na damu; yanaweza tu kusemekana kuwa maarifa na uzoefu wa mtu ambaye alikuwa ametiwa nuru na Roho Mtakatifu. Nikisema hivi namaanisha kwamba barua za Paulo si vitabu kutoka mbinguni. Barua hizi si takatifu, na hazikutamkwa ama kuonyeshwa na Roho Mtakatifu hata kidogo; ni maonyesho tu ya mzigo wa Paulo kwa ajili ya makanisa. Lengo Langu katika kusema haya yote ni kuwafanya muelewe tofauti kati ya kazi ya Mungu na kazi ya mwanadamu: Kazi ya Mungu inamwakilisha

Mungu Mwenyewe, wakati kazi ya mwanadamu inawakilisha wajibu na uzoefu wa mwanadamu. Mtu hapaswi kuchukulia kazi ya kawaida ya Mungu kama mapenzi ya mwanadamu na kazi Yake ya mwujiza kama mapenzi ya Mungu; aidha, mtu hapaswi kuyachukulia mahubiri ya kiburi ya mwanadamu kama matamshi ya Mungu ama kama vitabu kutoka mbinguni. Maoni yote kama haya hayana maadili. Wanaponisikia Nikichambua nyaraka kumi na tatu za Paulo, watu wengi wanaamini kwamba barua za Paulo hazipaswi kusomwa, na kwamba Paulo alikuwa mtu mwenye dhambi sana. Hata kuna watu wengi wanaofikiri maneno Yangu hayana huruma, kwamba makadirio Yangu ya nyaraka za Paulo si sahihi, na kwamba barua hizo hazipaswi kuchukuliwa kuwa maonyesho ya uzoefu na mzigo wa mwanadamu. Wanaamini kuwa badala yake zinapaswa kuchukuliwa kuwa maneno ya Mungu, kwamba ni muhimu kama Kitabu cha Yohana cha Ufunuo, kwamba haziwezi kufupishwa ama kuongezewa, na, aidha, haziwezi kueleza kwa kugusia juujuu. Je, madai haya yote ya binadamu hayana makosa? Je, hilo halijasababishwa na watu kutokuwa na busara kabisa? Barua za Paulo zinawafaidi watu sana, na tayari zina historia ya zaidi ya miaka 2,000. Hata hivyo, hadi leo, bado kuna watu wengi wasioweza kuelewa alichosema wakati huo. Watu huziona barua za Paulo kuwa kazi bora zaidi katika Ukristo wote, na kwamba hakuna mtu anayeweza kuzifumbua, na kwamba hakuna mtu anayeweza kuzielewa kikamilifu. Kwa kweli, barua hizi ni kama tu wasifu wa mtu wa kiroho, na haziwezi kulinganishwa na maneno ya Yesu ama maono makuu aliyoyaona Yohana. Kinyume chake, aliyoyaona Yohana yalikuwa maono makuu kutoka mbinguni—unabii wa kazi ya Mungu mwenyewe—ambayo hayakuweza kutimizwa na mwanadamu, ilhali barua za Paulo ni maelezo tu ya kile mwanadamu aliona na kupitia. Ni yale ambayo mwanadamu anaweza kutimiza, lakini si unabii wala maono; ni barua tu zilizotumwa maeneo mbalimbali. Hata hivyo, kwa watu wa wakati huo, Paulo alikuwa mfanyakazi, na kwa hiyo maneno yake yalikuwa na thamani, kwa sababu alikuwa mtu aliyekubali alichoaaminiwa. Kwa sababu ya hayo, barua zake ziliwanufaisha wale wote waliomtafuta Kristo. Ingawa maneno hayo hayakunenwa na Yesu binafsi, mwishowe yalikuwa na umuhimu kwa wakati wao. Kwa hiyo, watu waliokuja baada ya Paulo walipanga barua zake katika Biblia, hivyo kuziwezesha kupitishwa hadi leo. Je, mnaelewa Ninachomaanisha? Nawapa tu maelezo sahihi ya barua hizi, na kuzichambua bila kupinga manufaa na thamani zao kwa watu kama marejeleo. Ikiwa hampingi tu barua za Paulo baada ya kuyasoma maneno Yangu, ila kuzichukulia kuwa uzushi ama zisizo na thamani, basi inaweza tu kusemekana kwamba uwezo wenu wa kuelewa na vilevile umaizi wenu na jinsi mnavyoyaona mambo ni dhaifu sana; hakika haiwezi kusemekana kwamba maneno Yangu ni ya upendeleo kupita kiasi. Je, mnaelewa sasa? Mambo muhimu mnayopaswa kuelewa ni hali halisi ya kazi ya Paulo wakati huo na mazingira ambamo barua zake ziliandikwa. Ikiwa mna maoni sahihi kuhusu vipengele hivi, basi pia mtakuwa na maoni sahihi ya nyaraka za Paulo. Wakati uo huo, punde tu mnapoelewa kiini cha barua hizo, makadirio yenu ya Biblia yatakuwa sahihi, na kisha mtaelewa

kwa nini nyaraka za Paulo zimependwa sana na vizazi vya baadaye vya watu kwa miaka mingi mno, na vilevile kwa nini hata kuna watu wengi wanaomchukulia kuwa Mungu. Je, hamngefikiria hivyo pia ikiwa hamngeelewa?

Mtu ambaye si Mungu Mwenyewe hawezi kumwakilisha Mungu Mwenyewe. Kazi ya Paulo inaweza tu kusemekana kuwa sehemu ya maoni ya binadamu na sehemu ya nuru ya Roho Mtakatifu. Paulo aliyaandika maneno haya kutoka kwa mtazamo wa binadamu, akiwa na nuru kutoka kwa Roho Mtakatifu. Hili ni jambo la kawaida. Hivyo haingeepukika kwamba maneno yake yalichanganywa na uzoefu kiasi wa binadamu, na baadaye alitumia uzoefu wake binafsi kuwaruzuku na kuwasaidia ndugu zake wakati huo. Barua alizoandika haziwezi kuainishwa kama uchunguzi wa maisha, wala haziwezi kuainishwa kama wasifu ama ujumbe. Aidha, hazikuwa ukweli uliotendwa na kanisa wala amri za utawala za kanisa. Kama mtu aliyekuwa na mzigo—mtu aliyepewa kazi na Roho Mtakatifu—hili ni jambo ambalo lazima tu alifanye. Roho Mtakatifu akiwainua watu na kuwapa mzigo, lakini wasifanye kazi ya kanisa, na wasiweze kusimamia shughuli zake vizuri, ama kutatua shida zake zote vyema kabisa, basi hili linathibitisha kwamba watu hao hawatimizi wajibu wao vizuri. Kwa hivyo halikuwa jambo la ajabu sana kwa mtume kuweza kuandika barua wakati wa kazi yake. Hii ilikuwa sehemu ya kazi yake; alilazimika kuifanya. Lengo lake la kuandika barua halikuwa kuandika uchunguzi wa maisha ama wasifu wa kiroho, na hakika halikuwa ili kuwafungulia watakatifu njia nyingine mbadala. Badala yake, alifanya hilo ili kutimiza kazi yake mwenyewe na kuwa mtumishi mwaminifu kwa Mungu, ili aweze kujieleza kwa Mungu kwa kukamilisha kazi Alizomwaminia. Ilimlazimu awajibike kwa sababu yake na kwa sababu ya ndugu zake katika kazi yake, na ilimlazimu afanye kazi yake vizuri na azingatie masuala ya kanisa: Haya yote yalikuwa tu sehemu ya kazi yake.

Ikiwa mmepata ufahamu wa barua za Paulo, pia mtakuwa na fikira na makadirio sahihi kuhusu nyaraka za Petro na Yohana. Hamtawahi tena kuziona barua hizi kuwa vitabu kutoka mbinguni ambazo ni takatifu na zisizokiukwa, sembuse kumchukulia Paulo kuwa Mungu. Hata hivyo, kazi ya Mungu ni tofauti na kazi ya mwanadamu, na aidha, maonyesho Yake yanawezaje kuwa sawa na ya mwanadamu? Mungu ana tabia Yake Mwenyewe ya pekee, ilhali mwanadamu ana wajibu ambao anapaswa kutimiza. Tabia ya Mungu inaonyeshwa katika kazi Yake, ilhali wajibu wa mwanadamu unadhihirishwakatika uzoefu wa mwanadamu na kuonyeshwa katika kazi za mwanadamu. Kwa hiyo inakuwa dhahiri kupitia kazi inayofanywa iwapo jambo fulani ni maonyesho ya Mungu ama maonyesho ya mwanadamu. Halihitaji kufafanuliwa na Mungu Mwenyewe, wala halihitaji mwanadamu ajitahidi kushuhudia; aidha, halimhitaji Mungu Mwenyewe kumkandamiza mtu yoyote. Yote haya yanakuja kama ufunuo wa kawaida; hayalazimishwi wala silo jambo ambalo mwanadamu anaweza kuingilia kati. Wajibu wa

mwanadamu unaweza kujulikana kupitia uzoefu wake, na hauhitaji watu wafanye kazi yoyote ya ziada inayohusu uzoefu wao. Nafsi yote ya mwanadamu inaweza kufichuliwa wakati anapotimiza wajibu wake, wakati Mungu anaweza kuonyesha tabia Yake ya asili anapotekeleza kazi Yake. Ikiwa ni kazi ya mwanadamu basi haiwezi kufichika. Ikiwa ni kazi ya Mungu, basi haiwezekani hata zaidi kwa tabia ya Mungu kufichwa na yeyote, sembuse kudhibitiwa na mwanadamu. Hakuna mwanadamu anayeweza kusemekana kuwa Mungu, wala kazi na maneno yake kuonekana kuwa matakatifu ama kuchukuliwa kuwa yasiyobadilika. Mungu anaweza kusemekana kuwa mwanadamu kwa sababu Amejivika mwili, lakini kazi Yake haiwezi kuchukuliwa kuwa kazi ya mwanadamu ama wajibu wa mwanadamu. Aidha, matamshi ya Mungu na nyaraka za Paulo hayawezi kulinganishwa, wala hukumu na kuadibu kwa Mungu na maneno ya mwanadamu ya kuagiza kuzungumziwa kuwa sawa. Kwa hiyo, kuna kanuni zinazotofautisha kazi ya Mungu na kazi ya mwanadamu. Zinatofautishwa kulingana na viini vyao, sio kwa upana wa kazi ama ustadi wake wa muda. Watu wengi hufanya makosa ya kanuni kuhusiana na hili. Hii ni kwa sababu mwanadamu anaangalia mambo ya nje, ambayo anaweza kutimiza, ilhali Mungu anaangalia kiini, ambacho hakiwezi kuonekana na macho ya mwanadamu. Ukichukulia maneno na kazi ya Mungu kama wajibu wa mtu wa kawaida, na kuona kazi kubwa ya mwanadamu kama kazi ya Mungu aliyejivika mwili badala ya wajibu ambao mwanadamu anatimiza, je, basi hujakosea kimsingi? Barua na wasifu wa mwanadamu vinaweza kuandikwa kwa urahisi, lakini kwa msingi tu wa kazi ya Roho Mtakatifu. Hata hivyo, matamshi na kazi ya Mungu haviwezi kufanikishwa kwa urahisi na mwanadamu ama kutimizwa kwa hekima na fikira za binadamu, na watu hawawezi kuvieleza kikamilifu baada ya kuvichunguza. Masuala haya ya kimsingi yasipowaletea hisia yoyote, basi ni dhahiri kwamba imani yenu si ya kweli ama safi sana. Inaweza tu kusemekana kwamba imani yenu imejaa mashaka, na imekanganyikiwa na ni isiyo na maadili. Bila hata kuelewa masuala ya msingi kabisa ya Mungu na mwanadamu, je, imani kama hii haijakosa utambuzi kabisa? Paulo anawezaje kuwa mtu wa pekee aliyetumika katika historia yote? Anawezaje kuwa mtu wa pekee aliyewahi kulifanyia kanisa kazi? Anawezaje kuwa mtu wa pekee aliyeyaandikia makanisa kuwasaidia? Bila kujali ukubwa ama ushawishi wa kazi ya watu hawa, au hata matokeo ya kazi yao, je, si kanuni na dutu yote ya kazi kama hiyo ni sawa? Je, hakuna mambo kuihusu ambayo ni tofauti kabisa na kazi ya Mungu? Hata ingawa kuna tofauti dhahiri kati ya kila hatua ya kazi ya Mungu, na hata ingawa mbinu Zake nyingi za kazi si sawa kabisa, je, zote hazina asili na dutu moja tu? Kwa sababu hiyo, ikiwa mtu bado hajaelewa mambo haya sasa, basi hana mantiki hata kidogo. Baada ya kuyasoma maneno haya, mtu bado akisema kwamba barua za Paulo ni takatifu na zisizokiukwa na ni tofauti na wasifu wa mtu yeyote wa kiroho, basi mantiki ya mtu huyu si ya kawaida hata kidogo na mtu kama huyu bila shaka ni mtaalamu wa maandishi ambaye hana akili kabisa. Hata kama unampenda Paulo sana, huwezi kutumia hisia zako changamfu kwake

kugeuza ukweli wa mambo ama kukanusha kuwepo kwa ukweli. Aidha, kile ambacho Nimesema hakitupilii mbali kazi na barua zote za Paulo hata kidogo ama kukana kabisa thamani yao kama marejeleo. Bila kujali chochote, nia Yangu ya kuzungumza maneno haya ni ili mpate ufahamu mzuri na makadirio ya kutosha ya mambo na watu wote: Hili pekee ndilo mantiki ya kawaida; ni hili tu ndilo watu wenye haki walio na ukweli wanapaswa kujitayarisha nalo.

Mafanikio au Kushindwa Kunategemea Njia Ambayo Mwanadamu Hutembea

Watu wengi wanamwamini Mungu kwa ajili ya hatima yao ya baadaye au kwa ajili ya starehe ya muda mfupi. Kwa wale ambao hawajapitia ushughulikiaji wowote, imani kwa Mungu ni kwa ajili ya kuingia mbinguni, ili kupata tuzo. Sio ili kufanywa wawe na ukamilifu, au kutekeleza wajibu wa kiumbe wa Mungu. Ambayo ni kusema kwamba watu wengi hawamwamini Mungu ili watimize majukumu yao, au kukamilisha wajibu wao. Mara chache watu humwamini Mungu ili waishi maisha ya maana, wala hamna wale ambao wanaamini kwamba kwa kuwa mwanadamu yu hai, anapaswa ampende Mungu kwa kuwa ni sheria ya Mbinguni na kanuni ya dunia kufanya hivyo, na ni wito wa asili wa mwanadamu. Kwa njia hii, ingawa watu tofauti kila mmoja hufuatilia malengo yao binafsi, lengo la harakati zao na motisha yao yote ni sawa, na, zaidi ya hayo, kwa wengi wao, malengo yao ya ibada kwa kiasi kikubwa ni sawa. Katika kipindi cha elfu kadhaa za miaka iliyopita, waumini wengi wamekufa, na wengi wamekufa na kuzaliwa tena. Sio mtu mmoja au wawili ambao humtafuta Mungu, wala hata watu elfu moja au mbili, ilhali harakati ya wengi wa watu hawa ni kwa ajili ya matarajio yao wenyewe ama matumaini yao tukufu ya siku zijazo. Wale ambao ni waaminifu kwa Kristo ni wachache na nadra. Waumini wengi wanaomcha Mungu bado wamekufa wakiwa wametegwa na nyavu zao wenyewe, na zaidi ya hayo, idadi ya watu ambao wamekuwa washindi, ni ndogo mno. Hadi siku ya leo, sababu za watu kushindwa, au siri ya ushindi wao, bado haijulikani kwao. Wale ambao wamejawa na hamu ya kumtafuta Kristo bado hawajapata wakati wao wa ufahamu wa ghafla, hawajafikia kina cha mafumbo haya, kwa sababu hawajui. Ingawa wao wanafanya juhudi za mchwa katika harakati zao, njia ambayo wanatembelea ni njia ya kushindwa ambayo ilitembelewa na watangulizi wao, na si njia ya mafanikio. Kwa njia hii, bila kujali jinsi wanavyotafuta, je, si wao wanatembea katika njia ambayo inaelekea gizani? Je, si wanachopata ni matunda machungu? Ni vigumu vya kutosha kutabiri ikiwa watu ambao huiga wale waliofaulu katika nyakati za zamani hatimaye watapata utajiri au msiba. Uwezekano ni mbaya kiasi gani, basi, kwa watu ambao hutafuta kwa kufuata nyayo za wale ambao hawakufaulu? Je, si wao wana uwezekano mkubwa zaidi wa kutofaulu? Ni thamani gani iliyoko katika njia wanayoipitia? Je, wao si wanapoteza wakati wao? Bila kujali iwapo mtu hufaulu ama hufeli

katika harakati yake, kuna, kwa kifupi, sababu kwa nini wao wanafanya hivyo, na si kweli kuwa kufaulu kwao ama kushindwa kwao kunaamuliwa na kutafuta vyovyote watakavyo.

Mahitaji ya msingi ya imani ya mtu kwa Mungu ni kuwa ni sharti awe na moyo mwaminifu, na kwamba ajitolee mwenyewe, na kutii kwa kweli. Kile kigumu sana kwa mwanadamu ni kupeana mwili wake ili abadilishe na imani ya kweli, ambapo kupitia hii anaweza kupata ukweli mzima, na kutimiza wajibu wake kama kiumbe wa Mungu. Hili haliwezi kupatikana na wale ambao wanafeli, na halipatikani hata zaidi na wale ambao hawawezi kumpata Yesu. Kwa sababu mwanadamu si hodari kwa kujitolea mwenyewe kwa Mungu kabisa, kwa sababu mwanadamu hayuko tayari kutekeleza wajibu wake kwa Muumba, kwa sababu mwanadamu ameona ukweli lakini anauepuka na kutembea katika njia yake mwenyewe, kwa sababu mwanadamu daima anatafuta kwa kufuata njia ya wale walioshindwa, kwa sababu mwanadamu daima anaasi Mbingu, hivyo, mwanadamu daima hushindwa, huchukuliwa na hila za Shetani, na anakamatwa kwa hila na wavu wake. Kwa sababu mwanadamu hamjui Kristo, kwa sababu mwanadamu hana ustadi katika kuelewa na kushuhudia ukweli, kwa sababu mwanadamu ni wa kuabudu Paulo sana na mwenye tamaa nyingi ya mbinguni, kwa sababu mwanadamu daima anadai kuwa Kristo awe akimtii yeye na kuagiza kuhusu Mungu, hivyo mashujaa hao wakuu na wale ambao wamepitia mabadiliko mabaya ya dunia bado wamo na ubinaadamu, na bado hufa kwa kuadibu kwa Mungu. Yote Ninayoweza kusema kuhusu watu kama hawa ni kuwa wanakufa kifo cha kutisha, na athari yao—kifo chao—si bila haki. Je, si kushindwa kwao hakuvumiliki hata zaidi kwa sheria ya Mbinguni? Ukweli unatoka katika ulimwengu wa mwanadamu, na bado ukweli katika mwanadamu unapitishwa na Kristo. Unaanzia kwa Kristo, yaani, kutoka kwa Mungu mwenyewe, na hiki si kitu ambacho mwanadamu anaweza kufanya. Ilhali Kristo hutoa ukweli tu; Yeye haji kuamua ikiwa mwanadamu atafanikiwa katika harakati yake ya kufuata ukweli. Hivyo, kinachofuata ni kuwa mafanikio au kushindwa kwa kweli yote yanategemea harakati ya mwanadamu. Mafanikio au kushindwa kwa mwanadamu kwa kweli kamwe hakuna uhusiano na Kristo, lakini kwa mbadala kunategemea harakati yake. Hatima ya mwanadamu na mafanikio yake ama kushindwa haiwezi kurundikwa kichwani pa Mungu, ili Mungu mwenyewe afanywe wa kuibeba, kwa sababu sio jambo la Mungu mwenyewe, lakini linahusiana moja kwa moja na wajibu ambao viumbe wa Mungu wanapaswa kutekeleza. Watu wengi wana maarifa madogo ya harakati na hatima za Paulo na Petro, lakini watu hawajui lolote ila matokeo ya Petro na Paulo, na hawajui kuhusu siri ya mafanikio ya Petro, au mapungufu yaliyosababisha kushindwa kwa Paulo. Na kwa hivyo, kama ninyi hamwezi kabisa kuelewa kiini cha harakati zao basi harakati ya wengi wenu bila shaka haitafaulu, na hata kama wachache wenu watafaulu, bado hawatakuwa sawa na Petro. Ikiwa njia unayopitia katika kutafuta ni ya kweli, basi una matumaini ya mafanikio. Kama njia unayopitia katika kufuatilia ukweli ni mbaya, basi wewe milele hutaweza

kufanikiwa, na utakuwa na hatima sawa na Paulo.

Petro alikuwa mtu aliyefanywa mkamilifu. Ni baada tu ya kupitia kuadibu na hukumu, na hivyo kupata upendo safi kwa Mungu, ndipo alifanywa mkamilifu kabisa; njia ambayo alipitia ilikuwa ni njia ya kukamilishwa. Ambayo ni kusema kuwa, tangu hapo mwanzo kabisa, njia ambayo Petro alipitia ilikuwa ya haki, na motisha ya kumwamini Mungu ilikuwa sahihi, na kwa hivyo akawa mtu aliyekuwa amefanywa kamili na alifuata njia mpya ambayo mwanadamu kamwe hajawahi kuitembelea hapo awali. Hata hivyo, njia ambayo Paulo alitembea tangu mwanzo ilikuwa njia ya upinzani kwa Kristo, na ni kwa sababu tu Roho Mtakatifu alitaka kumtumia, na kufaidika na vipaji vyake na ustahili wake wote kwa kazi yake, kwamba alifanya kazi kwa ajili ya Kristo kwa miongo mingi. Alikuwa mtu tu ambaye alitumiwa na Roho Mtakatifu, na hakutumika kwa sababu Yesu alitazama ubinadamu wake kwa mapendeleo, lakini ni kwa sababu ya vipaji vyake. Aliweza kufanya kazi ya Yesu kwa sababu alipigwa, na sio kwa sababu alifurahia kufanya hivyo. Aliweza kufanya kazi kama hiyo kwa sababu ya kupata nuru na uongozi wa Roho Mtakatifu, na kazi aliyiofanya haikuwakilisha ufuatiliaji wake kwa njia yeyote, au ubinadamu wake. Kazi ya Paulo iliwakilisha kazi ya mtumishi, ambayo ni kusema kuwa yeye alifanya kazi ya mtume. Petro, hata hivyo, alikuwa tofauti: Yeye pia alifanya baadhi ya kazi; haikuwa kuu kama kazi ya Paulo, lakini alifanya kazi huku akiwa na harakati ya kuingia kwake mwenyewe, na kazi yake ilikuwa tofauti na kazi ya Paulo. Kazi ya Petro ilikuwa utekelezaji wa wajibu wa kiumbe wa Mungu. Yeye hakufanya kazi katika nafasi ya mtume, lakini alifanya kazi huku akifuatilia upendo kwa Mungu. Mwendo wa kazi ya Paulo pia ulikuwa na harakati yake binafsi. Ufuatiliaji wake ulikuwa tu kwa ajili ya matumaini yake ya siku za baadaye, na shauku yake ya hatima nzuri. Yeye hakukubali usafishaji wakati wa kazi yake, wala hakukubali upogoaji na ushughulikaji. Yeye aliamini kuwa alimradi kazi aliyiofanya iliridhisha mapenzi ya Mungu, na yote aliyofanya yalimpendeza Mungu, basi tuzo hatimaye ilikuwa inamsubiri. Hakukuwa na matukio ya kibinafsi katika kazi yake—yote yalikuwa kwa ajili yake mwenyewe, na hayakufanyika huku kukiwa na harakati ya mabadiliko. Kila kitu katika kazi yake kilikuwa shughuli, na hakukuwa na wajibu wowote au kujisalimisha kwa kiumbe cha Mungu. Wakati wa safari ya kazi yake, hakuna mabadiliko yaliyotokea katika tabia ya zamani ya Paulo. Kazi yake ilikuwa tu ya kufanya huduma kwa ajili ya wengine, na haikuwa na uwezo wa kuleta mabadiliko katika tabia yake. Paulo alifanya kazi yake moja kwa moja, bila ya kufanywa mkamilifu ama kushughulikiwa, na alivutiwa na thawabu. Petro alikuwa tofauti: alikuwa mtu ambaye alikuwa amepitia upogoaji na ushughulikaji na alikuwa amepitia usafishaji. Lengo na motisha za kazi ya Petro zilikuwa tofauti kimsingi na zile za Paulo. Ingawa Petro hakufanya sehemu kubwa ya kazi, tabia yake ilipitia mabadiliko mengi, na alichotafuta ni ukweli, na mabadiliko ya kweli. Kazi yake haikufanyika tu kwa ajili ya kazi yenyewe. Ingawa Paulo alifanya kazi nyingi, yote ilikuwa

kazi ya Roho Mtakatifu, na ingawa Paulo alishirikiana katika kazi hii, yeye, hakuipitia. Kwamba Petro alifanya kazi ndogo ilikuwa tu kwa ajili Roho Mtakatifu hakufanya kazi kubwa kupitia yeye. Wengi wa kazi zao haukuamua iwapo walikuwa wamefanywa wakamilifu; harakati ya mmoja ilikuwa ili kupokea tuzo, na ile ya mwingine ilikuwa ili kufikia upendo wa mwisho kwa Mungu na kutimiza wajibu wake kama kiumbe cha Mungu, kwa kiasi kwamba angeweza kuishi kwa kudhihirisha picha inayopendeza ili kukidhi mapenzi ya Mungu. Nje walikuwa tofauti, na pia vile vile viini vyao vilikuwa tofauti. Huwezi kuamua ni nani kati yao alifanywa mkamilifu kwa msingi wa kazi waliyofanya. Petro alitafuta kuishi kwa kudhihirisha picha ya yule ambaye hupenda Mungu, kuwa mtu ambaye alimtii Mungu, kuwa mtu ambaye alikubali ushughulikaji na upogoaji, na kuwa mtu aliyetekeleza wajibu wake kama kiumbe wa Mungu. Aliweza kujitolea kwa Mungu, kuweka nafsi yake kamilifu katika mikono ya Mungu, na kumtii hadi kifo. Hilo ndilo alilokuwa ameamua kufanya na, zaidi ya hayo, hilo ndilo alilotimiza. Hii ndiyo sababu ya msingi ya kwani hatima yake ilikuwa tofauti na ile ya Paulo. Kazi ambayo Roho Mtakatifu alifanya ndani ya Petro ilikuwa kumfanya mkamilifu, na kazi ambayo Roho Mtakatifu alifanya ndani ya Paulo ilikuwa kumtumia. Hii ni kwa sababu asili zao na mitazamo yao kuhusu harakati hazikuwa sawa. Wote walikuwa na kazi ya Roho Mtakatifu. Petro alitumia kazi hii kwake mwenyewe, na pia akawapa watu wengine; Paulo, kwa upande mwingine, aliwapa wengine kazi nzima ya Roho Mtakatifu, na mwenyewe hakufaidika na chochote kutoka kwa kazi hiyo. Kwa njia hii, baada ya yeye kushuhudia kazi ya Roho Mtakatifu kwa miaka mingi, mabadiliko ndani ya Paulo yalikuwa karibu na kutokuwepo. Yeye bado alibaki karibu katika hali yake ya asili, na bado yeye alikuwa yule Paulo wa awali. Ni baada tu ya kuvumilia ugumu wa miaka mingi ya kazi, ndivyo alikuwa amejifunza jinsi ya kufanya “kazi” na kujifunza uvumilivu, lakini asili yake ya zamani—ushindani wake mkuu na asili wa kimamluki—bado ilibaki. Baada ya kufanya kazi kwa miaka mingi, hakufahamu asili yake potovu, wala hakuwa amejiondoa mwenyewe kutoka kwa asili yake ya zamani, na bado ilikuwa inaonekana katika kazi yake. Kwake, kulikuwepo tu na uzoefu wa kazi zaidi, lakini uzoefu mdogo kiasi hicho pekee haukuwa na uwezo wa kumbadilisha na hukuweza kubadilisha maoni yake kuhusu kuwepo au umuhimu wa harakati yake. Ingawa alimfanyia Kristo kazi kwa miaka mingi, na hakumtesa tena Bwana Yesu, ndani ya Moyo wake hakukuwa na mabadiliko katika elimu kuhusu Mungu. Hii ina maana kuwa hakufanya kazi ili awe mwaminifu kwa Mungu, lakini badala yake, alilazimika kufanya kazi kwa ajili ya hatima yake ya siku zijazo. Kwa kuwa, hapo mwanzo, alimtesa Kristo, na hakumtii Kristo; kiasili yeye alikuwa mwasi ambaye alimpinga Kristo kimakusudi, na mtu ambaye hakuwa na elimu kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu. Kazi yake ilipokuwa inakaribia kukamilika, yeye bado hakujua kazi ya Roho Mtakatifu, na yeye tu alitenda kwa hiari yake mwenyewe kwa mujibu wa hulka yake mwenyewe, bila hata kidogo kutilia maanani mapenzi ya Roho Mtakatifu. Na hivyo asili yake ilikuwa katika uhasama na Kristo na haikutii ukweli. Mtu kama huyu,

ambaye alikuwa ameachwa na kazi ya Roho Mtakatifu, ambaye hakujua kazi ya Roho Mtakatifu, na ambaye pia alimpinga Kristo—je, ni jinsi gani mtu kama huyu angeokolewa? Iwapo mtu ataweza kuokolewa au la haitegemei kiasi cha kazi anayoifanya, au ni kiasi gani anajitolea, lakini badala yake kuamuliwa na iwapo anajua au hajui kazi ya Roho Mtakatifu, iwapo anaweza kuweka ukweli kwenye vitendo au la, na iwapo maoni yake kuhusu harakati yanalingana na ukweli au la.

Ingawa ufunuo wa asilia ulitokea baada ya Petro kuanza kumfuata Yesu, katika asili alikuwa, tangu mwanzo kabisa, mtu ambaye alikuwa tayari kujiwasilisha kwa Roho Mtakatifu na kumtafuta Kristo. Utiifu wake kwa Roho Mtakatifu ulikuwa safi: hakutafuta umaarufu na mali, lakini badala yake alikuwa amepewa motisha na utii wa ukweli. Ingawa kuna nyakati tatu ambapo Petro alikana kumjua Kristo, na ingawa alimjaribu Bwana Yesu, udhaifu kidogo kama huu wa kibinadamu haukubeba uhusiano wa asilia yake, na haukuathiri harakati zake za mbeleni, na huwezi kuthibitisha kikamilifu ya kuwa majaribu yake yalikuwa kitendo cha mpinga Kristo. Udhaifu wa kawaida wa kibinadamu ni kitu ambacho kimo kwa watu wote duniani—je, unatarajia Petro kuwa tofauti vyovyote vile? Je, si watu wana mtazamo fulani kuhusu Petro kwa sababu alifanya makosa mengi ya kijinga? Na je, si watu wanampenda Paulo kwa sababu ya kazi yote aliyoifanya, na nyaraka zote alizoandika? Itakuwaje mtu kuwa na uwezo wa kuona kupitia kiini cha mwanadamu? Hakika, je, wale ambao kwa kweli wana hisia wanaweza kuona kitu chenye thamani ndogo kama hiyo? Ingawa miaka mingi ya matukio ya uchungu ya Petro hayajanakiliwa katika Biblia, hii haithibitishi kuwa Petro hakuwa na matukio halisi, au kwamba Petro hakufanywa mkamilifu. Ni jinsi gani kazi ya Mungu inaweza kueleweka na mwanadamu? Kumbukumbu kwenye Biblia hazikuchaguliwa binafsi na Yesu, lakini zilikusanywa na vizazi vya baadaye. Kwa njia hii, si yote ambayo yaliandikwa katika Biblia yalichaguliwa kulingana na mawazo na mwanadamu? Zaidi ya hayo, hatima ya Petro na Paulo hazijaelezwa kwa dhati katika nyaraka, kwa hivyo mwanadamu anawahukumu Petro na Paulo kulingana na mtazamo wake mwenyewe, na kulingana na matakwa yake mwenyewe. Na kwa kuwa Paulo alifanya kazi kubwa sana, kwa sababu “michango” yake ilikuwa mikuu sana, yeye alipata imani ya umma. Je, si mwanadamu anamakinika tu na vitu vya juu juu tu. Inakuwaje mwanadamu kuwa na uwezo wa kuona kupitia kwa kiini cha mwanadamu? Bila kutaja, kwa kuwa Paulo amekuwa mlengwa wa ibada kwa maelfu ya miaka, ni nani ambaye atathubutu kukana kazi yake kwa haraka? Petro alikuwa mvuvi tu, hivyo ni jinsi gani mchango wake ungekuwa mkubwa kama ule wa Paulo? Kwa msingi wa mchango, Paulo angepaswa kuzawadiwa kabla ya Petro, na inapaswa kuwa yeye ndiye angekuwa amehitimu vyema zaidi kupata kibali cha Mungu. Nani angeweza kufikiri kuwa, katika kumtendea Paulo, Mungu alimfanya tu afanye kazi kupitia vipawa vyake, ilhali Mungu alimfanya Petro kuwa mkamilifu. Si kwa njia yoyote kweli ya kwamba Bwana Yesu alikuwa

amefanya mpango kwa ajili ya Petro na Paulo tangu mwanzo kabisa: Badala yake, walifanywa wakamilifu au kuwekwa kazini kulingana na tabia zao za kiasili. Na kwa hivyo, kitu ambacho wanadamu wanachoona kama michango ya nje ya mwanadamu tu, ilhali anachoona Mungu ni kiini cha mtu, na vile vile kama njia ambayo mwanadamu hufuatilia tangu mwanzo, na motisha inayosukuma harakati ya mwanadamu. Watu hupima mwanadamu kulingana na dhana zao, na kulingana na mitazamo yao wenyewe, na bado hatima ya mwisho ya mwanadamu haiamuliwi kulingana na mambo ya nje ya mwanadamu. Na kwa hivyo Mimi ninasema kwamba kama njia unayochukua tangu mwanzo ni njia ya mafanikio, na mtazamo wako kuhusu harakati ni sahihi tangu mwanzo, basi wewe ni kama ya Petro; kama njia ambayo unatembea ni njia ya kushindwa, basi gharama yoyote ambayo unalipa, hatima yako itakuwa sawa na ile ya Paulo. Yawayo yoyote, hatima yako, na kama utafaulu ama hautafaulu, yote yanaamuliwa na kama njia unayotafuta ni sahihi ama si sahihi, badala ya kujitolea kwenu, au gharama ambayo wewe hulipa. Kiini cha Petro na kiini cha Paulo, na malengo ambayo walifuatilia, yalikuwa tofauti; mwanadamu hana uwezo wa kugundua vitu hivi, na Mungu pekee anaweza kuyajua kwa ujumla wao. Kwa kuwa kitu ambacho Mungu huona ni kiini cha mwanadamu, ilhali mwanadamu hajui chochote kuhusu kiini chake mwenyewe. Mwanadamu hana uwezo wa kukitazama kiini ndani ya mwanadamu ama kimo chake halisi, na hivyo hana uwezo wa kutambua sababu za kutofaulu ama kufaulu kwa Paulo na Petro. Sababu ya wanadamu wengi kumuabudu Paulo na wala si Petro ni kuwa Paulo alitumika katika kazi ya umma, na mwanadamu anaweza kutambua kazi hii, na hivyo watu wanakiri “mafanikio” ya Paulo. Matukio ya Petro, wakati huo huo, hayaonekani na mwanadamu, na kwamba kile alichotafuta hakipatikani na mwanadamu, na hivyo mwanadamu hana moyo wa kutaka kumjua Petro.

Petro alifanywa mkamilifu kwa kupitia ushughulishaji na usafishaji. Alisema, “Mimi ni lazima nikidhi mapenzi ya Mungu wakati wote. Kwa yote nifanyayo mimi natafuta tu kukidhi mapenzi ya Mungu, na kama mimi ninaadibiwa, au kuhukumiwa, bado nina furaha kufanya hivyo.” Petro alimpa Mungu kila kitu chake, na kazi yake, maneno, na maisha yote yalikuwa yote kwa ajili ya kumpenda Mungu. Alikuwa mtu ambaye alitafuta utakatifu, na alipopitia zaidi, ndivyo upendo wake wa Mungu ndani ya moyo wake ulikuwa mkubwa zaidi. Paulo, wakati huo huo, alifanya tu kazi ya nje, na ingawa alitia bidii katika kazi yake, juhudi zake zilikuwa kwa ajili ya kufanya kazi yake vizuri na hivyo kupata tuzo. Angalijua kuwa hatapokea tuzo, yeye angalikata tamaa katika kazi yake. Kitu ambacho Petro alijali mno ni upendo wa kweli moyoni mwake, na ule ambao ulikuwa wa vitendo na ungeweza kutimizika. Yeye hakujali kuhusu iwapo angepokea tuzo, lakini kuhusu iwapo tabia yake ingebadilishwa. Paulo alijali kuhusu kufanya kazi kwa bidii hata zaidi, yeye alijali kuhusu kazi ya nje na kujitolea, na kuhusu mafundisho ambayo hayashuhudiwi na watu wa kawaida. Yeye hakujali chochote kuhusu mabadiliko ndani

yake wala kwa ajili ya upendo wa kweli kwa Mungu. Uzoefu wa Petro ulikuwa kwa ajili ya kupata upendo wa kweli na maarifa ya kweli kuhusu Mungu. Uzoefu wake ulikuwa ili kupata uhusiano wa karibu na Mungu, na kwa kuishi kwa kudhihirisha kwa vitendo. Kazi ya Paulo ilifanywa kwa sababu ya kile alichuaminiwa na Yesu, na ili apate vitu ambavyo alitamani, lakini haya hayakuwa na uhusiano na elimu yake mwenyewe na ya Mungu. Kazi yake ilikuwa tu kwa ajili ya kuepuka kuadibu na hukumu. Kitu ambacho Petro alitafuta kilikuwa ni upendo safi, na Paulo alitafuta taji ya hali ya kuwa mwenye haki. Petro alishuhudia miaka mingi ya kazi ya Roho Mtakatifu, na alikuwa na elimu ya vitendo kuhusu Kristo, na vile vile elimu ya kina kujihusu yeye mwenyewe. Na hivyo, upendo wake wa Mungu ulikuwa safi. Miaka mingi ya usafishaji ilikuwa imeinua elimu yake kuhusu Yesu na maisha, na upendo wake ulikuwa upendo usio na masharti, ulikuwa upendo wa hiari, na hakuagiza chochote akitarajia malipo, na wala hakutumainia kuwa na faida yeyote. Paulo alifanya kazi kwa miaka mingi, ilhali hakumiliki elimu kubwa ya Yesu, na elimu yake ya kibinafsi ilikuwa ndogo mno. Yeye kwa kifupi hakuwa na upendo kwa Kristo, na kazi yake na mwendo ambao alikimbia ilikuwa ili apate heshima na taji la mwisho. Kitu ambacho alitafuta kilikuwa taji zuri kabisa, wala si upendo safi. Yeye hakutafuta kikamilifu, lakini kwa kutoonyesha hisia; hakuwa anatekeleza majukumu yake, lakini alilazimika katika harakati yake baada ya kukamatwa na kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa hivyo, harakati yake haithibitishi kuwa yeye alikuwa kiumbe wa Mungu kilichokuwa na sifa zinazostahili; ilikuwa ni Petro ambaye alikuwa kiumbe wa Mungu aliyekuwa na sifa zilizostahili na ambaye alitekeleza wajibu wake. Mwanadamu anafikiri kuwa wale wote wanaotoa mchango kwa Mungu wanapaswa kupokea tuzo, na kwamba mchango unavyokuwa mkubwa zaidi, ndivyo mwanadamu anavyosadiki zaidi kuwa atapokea fadhila za Mungu. Kiini cha mtazamo wa mwanadamu ni wa shughuli, na hatafuti kikamilifu kutekeleza wajibu wake kama kiumbe wa Mungu. Kwa Mungu, watu wanavyozidi kutafuta upendo kwa Mungu wa kweli na utii mkamilifu kwa Mungu, ambayo pia ina maana kutafuta kutekeleza wajibu wao kama viumbe wa Mungu, ndivyo zaidi wanaweza kupata kibali cha Mungu. Mtazamo wa Mungu ni kudai kwamba mwanadamu arejeshe hadhi na wajibu wake wa awali. Mwanadamu ni kiumbe wa Mungu, na kwa hivyo mwanadamu hapaswi kuvuka mpaka mwenyewe kwa kutoa madai yoyote kwa Mungu, na anapaswa asifanye lolote zaidi ya kutekeleza wajibu wake kama kiumbe wa Mungu. Hatima ya Paulo na hatima ya Petro ilipimwa kulingana na iwapo wangeweza kutekeleza wajibu wao kama viumbe wa Mungu, na wala si kulingana na ukubwa wa mchango yao; hatima zao ziliamuliwa kulingana na kile ambacho walitafuta tangu mwanzo, wala si kulingana na kiasi cha kazi waliyofanya, au makadirio ya watu wengine kuwahusu. Kwa hivyo, kutafuta kutekeleza kikamilifu wajibu wa mtu kama kiumbe wa Mungu ndiyo njia ya mafanikio; kutafuta njia ya upendo wa kweli kwa Mungu ndiyo njia sahihi kabisa; kutafuta mabadiliko katika tabia ya zamani ya mtu, na kutafuta upendo safi kwa Mungu, ndiyo njia ya mafanikio. Njia kama hii ya

mafanikio ndiyo njia ya kurejeshwa kwa wajibu wa awali na vile vile pia kuonekana kwanza kwa kiumbe wa Mungu. Hiyo ndiyo njia ya kurejeshwa, na pia ni lengo la kazi yote ya Mungu kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kama harakati ya mwanadamu inatiwa doa na madai badhirifu ya kibinafsi na tamaa isiyo ya akili, basi athari ambayo inatimizwa haitakuwa mabadiliko katika tabia ya mwanadamu. Hii ni kinyume na kazi ya kurejeshwa. Bila shaka siyo kazi inayofanywa na Roho Mtakatifu, na hivyo hii inathibitisha kuwa harakati ya aina hii haikubaliki na Mungu. Harakati ambayo haijakubalika na Mungu ina umuhimu gani?

Kazi iliyofanywa na Paulo ilionyeshwa mbele ya mwanadamu, lakini upendo wake wa Mungu ulikuwa safi kiasi gani, upendo wake kwa Mungu ulikuwa ndani ya moyo wake kiasi gani—haya hayaonekani na mwanadamu. Mwanadamu anaweza tu kutazama kazi ambayo aliifanya, ambapo mwanadamu hujua kuwa kwa hakika alitumika na Roho Mtakatifu, na hivyo mwanadamu hudhani kwamba Paulo alikuwa bora kuliko Petro, ya kwamba kazi yake ilikuwa kubwa zaidi, kwa kuwa alikuwa na uwezo wa kutoa kwa makanisa. Petro alitazama tu matukio yake binafsi, na akapata watu wachache wakati wa kazi yake ya mara kwa mara. Kutoka kwake kunazo lakini nyaraka chache zinazojulikana, lakini ni nani anayejua jinsi upendo wa Mungu ulivyokuwa mkubwa kiasi gani moyoni mwake? Siku zote, usiku na mchana, Paulo alimfanyia Mungu kazi: alimradi kulikuwepo na kazi ya kufanywa, yeye aliifanya. Yeye alihisi kuwa kwa njia hii angeweza kulipata taji, na angemridhisha Mungu, lakini hakutafuta njia za kujibadilisha mwenyewe kupitia kazi hii. Chochote katika maisha ya Petro ambacho hakikukimu mapenzi ya Mungu kilimfanyia kuhisi wasiwasi. Kama hakikukidhi mapenzi ya Mungu, basi angehisi kujuta, na angetafuta njia mwafaka ambayo angejitahidi kuridhisha moyo wa Mungu. Hata katika masuala madogo kabisa maishani mwake yasiyokuwa na maana, bado alijishurutisha mwenyewe kukidhi mapenzi ya Mungu. Alikuwa pia mkali ilipofikia tabia yake ya asili na alikuwa daima mkali katika masharti yake mwenyewe ili kuelekea ndani zaidi kwa ukweli. Paulo alitafuta tu sifa na hadhi ya kijuu juu. Alitafuta kuringa mwenyewe mbele za mwanadamu, na hakutafuta kufanya maendeleo zaidi katika kuingia kwa maisha. Kile alichojali kuhusu ni mafundisho ya kidini, si uhalisi. Baadhi ya watu husema, “Paulo alimfanyia Mungu kazi nyingi, kwa nini yeye hakukumbukwa na Mungu? Petro alimfanyia Mungu kazi kidogo, na hakufanya mchango mkubwa katika makanisa, je, kwa nini yeye alifanywa mkamilifu?” Petro alimpenda Mungu hadi kiwango fulani, ambacho kilitakiwa na Mungu; ni watu kama hawa pekee wana ushuhuda. Na kuhusu Paulo? Ni kiwango gani ambacho Paulo alimpenda Mungu, je, wewe wajua? Kazi ya Paulo ilikuwa kwa ajili ya nini? Na kazi ya Petro ilikuwa kwa ajili ya nini? Petro hakufanya kazi kubwa, lakini, je, wafahamu ni nini kilikuwa moyoni mwake? Kazi ya Paulo inahusiana na utoaji makanisani, na msaada wa makanisa. Kile ambacho Petro alishuhudia ni mabadiliko ya tabia ya maisha yake; alishuhudia upendo kwa Mungu. Kwa kuwa sasa unajua tofauti katika kiini cha

kila mmoja wao, unaweza kuona ni nani, hatimaye, kwa kweli alimwamini Mungu, na ni nani ambaye kwa kweli hakumwamini Mungu. Mmoja wao alimpenda Mungu kwa kweli, na mwingine hakupenda Mungu kwa kweli; mmoja alipitia mabadiliko katika tabia yake, na mwingine hakupitia; mmoja alihudumu kwa unyenyekevu, na hakuonekana na watu kwa urahisi na mwingine aliabudiwa na watu, na alikuwa na picha nzuri; mmoja alitafuta utakatifu, na mwingine hakuutafuta, na ingawa hakuwa najisi, hakuwa amemilikiwa na upendo safi; mmoja alimilikiwa na ubinadamu wa kweli, na mwingine hakuwa nao; mmoja alikuwa na hisia ya kiumbe wa Mungu, na mwingine hakuwa na hisia hiyo. Tofauti kama hizi ndizo zilizo katika kiini cha Paulo sawa na Petro. Njia ambayo Petro alitembea ni njia ya mafanikio, ambayo pia ni njia ya kutimiza kupatwa tena kwa ubinadamu wa kawaida na wajibu wa kiumbe wa Mungu. Petro anawakilisha wote hao waliofaulu. Njia ambayo Paulo aliitembea ni njia ya kushindwa, na anawakilisha wale wote ambao wanajisalimisha na kujipa matarajio yao wenyewe ya kijuu juu, na hawampendi Mungu kwa dhati. Paulo anawakilisha wote ambao hawana ukweli. Katika imani yake kwa Mungu, Petro alitafuta kumridhisha Mungu katika kila kitu, na alitafuta kutii yote yaliyotoka kwa Mungu. Bila malalamiko hata kidogo, aliweza kukubali kuadibu na hukumu, na vile vile usafishaji, dhiki na kuwa bila kitu maishani, yote ambayo hayangeweza kubadilisha upendo wake kwa Mungu. Je, huu haukuwa upendo mkamilifu kwa Mungu? Je, huku hakukuwa ni kutimiza wajibu wa kiumbe wa Mungu? Kuadibu, hukumu, dhiki—una uwezo wa kufikia utii hadi kifo, na hili ndilo linafaa kutimizwa na kiumbe wa Mungu, huu ni usafi wa upendo kwa Mungu. Kama mwanadamu anaweza kutimiza kiasi hiki, basi yeye ni kiumbe wa Mungu mwenye sifa inayostahili, na hakuna kitu kinachokidhi mapenzi ya Muumba bora zaidi ya hiki. Fikiria kwamba wewe unaweza kumfanyia Mungu kazi, ilhali wewe humtii Mungu, na huna uwezo wa kumpenda Mungu kwa kweli. Kwa njia hii, wewe hutakuwa tu umekosa kutimiza wajibu wa kiumbe cha Mungu, lakini pia utalaaniwa na Mungu, kwa kuwa wewe ni mtu ambaye hana ukweli, ambaye hana uwezo wa kumtii Mungu, na ambaye si mtiifu kwa Mungu. Wewe unajali tu kuhusu kumfanyia Mungu kazi, na hujali kuhusu kuweka ukweli katika vitendo, ama kujifahamu. Wewe humfahamu ama kumjua Muumba, na humtii ama kumpenda Muumba. Wewe ni mtu ambaye asilia si mtiifu kwa Mungu, na hivyo watu kama hawa hawapendwi na Muumba.

Baadhi ya watu husema, “Paulo alifanya kazi kubwa kiasi cha ajabu, na alibeba mizigo mikubwa ya makanisa na aliwachangia mno. Nyaraka kumi na tatu ya Paulo zilizingatia miaka 2,000 ya Enzi ya Neema, na ni za pili tu baada ya Injili Nne. Nani anaweza kulinganishwa naye? Hakuna ambaye anaweza kufumbua maandiko ya Ufunuo wa Yohana, ilhali nyaraka za Paulo zinatoa maisha, na kazi ambayo alifanya ilikuwa na manufaa kwa makanisa. Ni nani mwingine angeweza kutimiza mambo kama haya? Na kipi ambacho Petro alikifanya?” Mwanadamu

anapowapima wengine, ni kwa mujibu wa michango yao. Mungu anapompima mwanadamu, ni kwa mujibu wa asili yake. Miongoni mwa wale ambao hutafuta uzima, Paulo alikuwa mtu ambaye hakujua kiini chake mwenyewe. Hakuwa kwa njia yoyote mnyenyekevu ama mtiifu, wala kujua kiini chake, ambacho kilikinzana na Mungu. Na kwa hivyo, alikuwa mtu ambaye hakuwa amepitia matukio ya kina, na alikuwa mtu ambaye hakuweka ukweli katika vitendo. Petro alikuwa tofauti. Yeye alijua kutokamilika kwake, udhaifu, na tabia yake potovu kama kiumbe wa Mungu, na hivyo alikuwa na njia ya vitendo ambayo angebadilishia tabia yake; hakuwa mmoja wa wale ambao walikuwa tu na mafundisho ya kidini lakini hawakuwa na uhalisi. Wale ambao hubadilika ni watu wapya ambao wameokolewa, ni wale ambao wana sifa zinazostahili katika kufuatilia ukweli. Watu ambao hawabadiliki ni wa wale ambao hawafai kwa sasa kiasili; ni wale ambao hawajaokolewa, yaani, ni wale ambao wamechukiwa na kukataliwa na Mungu. Hawatakumbukwa na Mungu bila kujali jinsi kazi zao ni kubwa. Wakati unapolinganisha haya na harakati yako mwenyewe, kama wewe hatimaye ni mtu wa aina sawa na Petro au Paulo inapaswa kuwa dhahiri kibinafsi. Kama bado hakuna ukweli kwa yale unayotafuta, na kama hata leo bado wewe ni mwenye kiburi na jeuri kama Paulo, na bado wewe ni mwepesi wa kusema maneno matupu na mwenye kujisifu kama yeye, basi bila shaka wewe ni aliyeharibika tabia na ambaye hushindwa. Kama wewe hutafuta jinsi sawa na Petro, kama unatafuta vitendo na mabadiliko ya kweli, na usiwe mwenye kiburi au mkaidi, bali utafute kutekeleza majukumu yako, basi utakuwa kiumbe wa Mungu ambaye anaweza kufikia ushindi. Paulo hakujua kiini chake mwenyewe ama upotovu, vile vile hakujua kutotii kwake. Hakuwahi kutaja uasi wake kwa Kristo unaostahili dharau, wala yeye hakuwa mwenye kujuta kupindukia. Yeye tu alipeana maelezo mafupi, na, ndani katika moyo wake, hakujiwasilisha kwa Mungu kikamilifu. Ingawa alianguka barabarani akielekea Dameski, yeye hakuangalia nafsi yake kwa kina. Aliridhika tu kwa kuendelea kufanya kazi, na hakuzingatia kujijua mwenyewe na kubadilisha tabia yake ya zamani kuwa jambo la muhimu zaidi ya masuala yote. Yeye aliridhika tu kwa kusema ukweli, na kukimu wengine kama dawa ya dhamiri yake mwenyewe, na kwa kutowatesa tena wanafunzi wa Yesu kujifariji na kujisamehe kwa dhambi zake za zamani. Lengo ambalo yeye alifuatilia tu lilikuwa taji ya wakati ujao na kazi ya muda pekee, lengo ambalo alifuatilia lilikuwa neema tele. Yeye hakutafuta ukweli wa kutosha, wala hakutafuta kuendelea ndani katika kiini cha ukweli ambao hakuwa hapo awali ameufahamu. Na kwa hivyo elimu yake ya nafsi yake inaweza semwa kuwa ya uwongo, na hakukubali kuadibu au hukumu. Kwamba aliweza kufanya kazi haina maana alikuwa na elimu ya asili yake au kiini; lengo lake lilikuwa la vitendo vya nje pekee. Lile ambalo daima alijitahidi kwalo, zaidi ya hayo, halikuwa mabadiliko, laikini elimu. Kazi yake kwa ujumla ilikuwa matokeo ya kuonekana kwa Yesu njiani kuelekea Dameski. Hakikuwa kitu ambacho alikuwa ameamua kukifanya hapo awali, wala haikuwa kazi ambayo ilikuwa imetokea baada ya yeye kukubali upogoaji wa tabia yake ya zamani. Bila kujali

jinsi ambavyo alifanya kazi, tabia yake ya zamani haikubadilika, na hivyo kazi yake haikulipia dhambi yake ya zamani lakini ilikuwa tu na wajibu fulani kwenye makanisa ya wakati huo. Kwa mtu kama huyu, ambaye tabia yake ya zamani haikubadilika—hivyo ni kusema, ambaye hakupata wokovu, na hata zaidi alikuwa bila ukweli—alikuwa hawezi kabisa kukuwa mmoja wa wale waliokubaliwa na Bwana Yesu. Hakuwa mtu ambaye alikuwa amejazwa na upendo na heshima kwa Yesu Kristo, wala hakuwa mtu ambaye alikuwa na ustadi katika kutafuta ukweli, na wala hakuwa mtu ambaye alitafuta fumbo la kupata mwili kwa Yesu Kristo. Alikuwa tu mtu ambaye alikuwa na ujuzi katika utata, na ambaye hangeweza kusalimu amri kwa yeyote ambaye alikuwa mkuu kwake au aliyekuwa na ukweli. Aliwaonea kijicho watu ama ukweli ambao ulikuwa tofauti naye, ama wenye uadui naye, na kupendelea watu wenye vipawa ambao walionyesha picha nzuri na kumiliki maarifa makubwa. Hakupenda kuingiliana na watu maskini ambao walitafuta njia ya ukweli na waliojali kuhusu ukweli pekee, na badala yake alijihusisha na viongozi mashuhuri kutoka mashirika ya kidini ambao walizungumza kuhusu mafundisho ya dini pekee, na walikuwa na elimu tele. Hakuwa na upendo wa kazi mpya ya Roho Mtakatifu, na hakujali kuhusu harakati za kazi mpya ya Roho Mtakatifu. Badala yake, yeye alipendelea kanuni hizo na mafundisho ya dini ambayo yalikuwa juu kuliko ukweli wa ujumla. Katika kiini chake cha kiasilia na uzima wa kile alichotafuta, hastahili kuitwa Mkristo ambaye alifuatilia ukweli, wala mtumishi mwaminifu katika nyumba ya Mungu, kwa kuwa unafiki wake ulikuwa mwingi sana, na kutotii kwake kulikuwa kukubwa sana. Ingawa anajulikana kama mtumishi wa Bwana Yesu, hakustahili kamwe kuingia kwenye lango la ufalme wa mbinguni, kwa kuwa matendo yake tangu mwanzo hadi mwisho hayawezi kuitwa yenye haki. Anaweza tu kuonekana kama mtu ambaye alikuwa mnafiki, na aliyefanya udhalimu, ilhali ambaye alimfanyia Yesu kazi. Ingawa hawezi kuitwa mwovu, yeye anaweza ipasavyo kuitwa mtu ambaye alifanya udhalimu. Alifanya kazi nyingi, ilhali ni lazima asihukumiwe juu ya wingi wa kazi aliyofanya, lakini tu kwa ubora na umuhimu wa kazi hiyo. Ni kwa njia hii tu ndiyo inawezekana kufikia kwenye kiini cha suala hili. Yeye siku zote aliamini: “Mimi nina uwezo wa kufanya kazi, mimi ni bora kuliko watu wengi; mimi ni mwenye kujali kuhusu mzigo wa Bwana kuliko mtu yeyote, na hakuna anayetubu sana kama ninavyotubu, kwa kuwa mwanga mkuu uling’aa kwangu, na nimeuona mwanga mkuu, na hivyo toba yangu ni kuu kuliko ya yeyote mwingine.” Wakati huo, hivi ndivyo alivyofikiria moyoni mwake. Mwishoni mwa kazi yake, Paulo alisema: “Nimefanya bidii katika mashindano, nimemaliza safari yote na sasa imebakia tu kupewa tuzo la ushindi kwa maisha ya uadilifu.” Mapambano yake, kazi, na safari zilikuwa kwa ajili ya taji la haki, na yeye hakusonga mbele; ingawa yeye hakuwa wa juu juu tu katika kazi yake, inaweza kusemwa kuwa kazi yake ilikuwa kwa ajili tu ya kusahihisha makosa yake, na kusahihisha shutuma za dhamiri yake. Yeye tu alitumaini kukamilisha kazi yake, kumaliza safari yake, na kupigana vita vyake haraka iwezekanavyo, ili kwamba aweze kupata tuzo lake la haki alilotamani kwa haraka.

Alilotamani halikuwa kukutana na Bwana Yesu na uzoefu wake na elimu ya kweli, lakini kukamilisha kazi yake haraka iwezekanavyo, ili kwamba aweze kupokea tuzo ambayo kazi yake ilikuwa imemwezesha kupata wakati alipokutana na Bwana Yesu. Alitumia kazi yake kujifariji, na kufanya makubaliano kwa ajili ya kupewa taji siku zijazo. Alichotafuta sio ukweli ama Mungu, lakini taji tu. Harakati kama hii inawezekanaje kuwa ya kiwangozezi? Motisha yake, kazi yake, gharama aliyolipa, na juhudi zake zote—ndoto zake za ajabu zilienea kote, na alifanya kazi kabisa kulingana na mapenzi yake. Katika ukamilifu wa kazi yake, hapakuwa na hiari kidogo ya gharama aliyolipa; alikuwa anashiriki kwenye mapatano tu. Juhudi zake hazikufanywa kwa hiari ili kutimiza wajibu wake, bali zilifanywa kwa hiari ili kutekeleza lengo la mapatano. Je, kuna thamani yoyote kwa jitihada kama hizo? Nani ambaye anaweza kusifu juhudi zake chafu? Nani ambaye ana moyo wa kujua juhudi kama hizi? Kazi yake ilijawa na ndoto za mbeleni, zilijawa na mipango ya ajabu, na hazikuwa na njia ya kubadilishia tabia ya kibinadamu. Ukirimu wake mwingi ulikuwa wa unafiki; kazi yake haikuleta maisha, lakini ilikuwa unyenyekevu bandia; lilikuwa tendo la maafikiano. Jinsi gani kazi kama hii kumwongoza mwanadamu kwenye njia ya kupata tena wajibu wake wa awali?

Yote ambayo Petro alitafuta yalikuwa kufuata Moyo wa Mungu. Alitaka kutimiza mapenzi ya Mungu, na licha ya taabu na mashaka, bado yeye alikuwa tayari kutimiza mapenzi ya Mungu. Hakuna ukimbizaji mkuu zaidi wa muumini katika Mungu. Kile ambacho Paulo alitafuta kilitiwa doa na mwili wake, na dhana zake mwenyewe, na mipango na mipangilio yake mwenyewe. Hakuwa kwa njia yeyote kiumbe wa Mungu aliyehitimu, hakuwa mtu ambaye alitaka kutimiza mapenzi ya Mungu. Petro alitaka kujiwasilisha kwenye mipango ya Mungu, na ingawa kazi aliyofanya haikuwa kuu, motisha ya harakati yake na njia ambayo alitembea zilikuwa sahihi; ingawa hakuweza kupata watu wengi, aliweza kufuata njia ya ukweli. Kwa hivyo inaweza kusemwa kwamba alikuwa kiumbe wa Mungu aliyehitimu. Leo, hata kama wewe si mfanyikazi, unapaswa kuwa na uwezo wa kutekeleza wajibu wa kiumbe wa Mungu, na kutafuta kujiwasilisha kwa mipango yote ya Mungu. Unapaswa kuwa na uwezo wa kutii chochote Mungu anachosema, na upitie kila aina ya madhila na usafishaji, na ingawa wewe ni dhaifu, moyoni mwako unapaswa bado uwe na uwezo wa kumpenda Mungu. Wale ambao huchukua jukumu katika maisha yao wako tayari kutekeleza wajibu wa kiumbe wa Mungu, na mtazamo wa watu kama hawa kuhusu harakati ni ule sahihi. Hawa ndio watu ambao Mungu anahitaji. Iwapo ulifanya kazi nyingi, na watu wengine walipata mafundisho yako, lakini wewe mwenyewe hukubadilika, na hukuwa na ushuhuda wowote, au kuwa na uzoefu wowote wa kweli, kwa namna kuwa katika hatima ya maisha yako, bado hakuna yoyote uliyofanya iliyo na ushuhuda, basi je, wewe ni mtu aliyebadilika? Je, wewe ni mtu ambaye hufuatilia ukweli? Wakati huo, Roho Mtakatifu alikutumia, lakini alipokutumia, alitumia sehemu yako ambayo ingeweza

kutumika kufanya kazi, na wala hakutumia sehemu yako ambayo haingeweza kutumika kufanya kazi. Kama wewe ulitafuta kubadilika, basi ungeweza kufanywa mkamilifu hatua kwa hatua wakati wa mchakato wa kutumika. Hata hivyo Roho Mtakatifu hakubali jukumu la kama au la wewe mwishowe utapatwa, na hii inategemea na namna ya ukimbizaji wako. Iwapo hakuna mabadiliko katika tabia yako binafsi, basi hiyo ni kwa sababu mtazamo wako kuelekea kufuatilia ni mbaya. Kama hutatunukiwa tuzo, basi hilo ni tatizo lako, na kwa sababu wewe mwenyewe hujaweka ukweli katika vitendo, na huwezi kutimiza mapenzi ya Mungu. Na kwa hivyo, hakuna kitu cha umuhimu kama uzoefu wako wa kibinafsi, na hakuna kilicho cha maana kuliko kuingia kwako kibinafsi. Baadhi ya watu wataishia kusema, “Mimi nimefanya kazi nyingi kwa ajili yako, na ingawa kuna uwezekano kuwa hazikuwa na mafanikio ya kusherehekeka, bado nimekuwa mwenye jitihada kwenye juhudi zangu. Huwezi tu kuniruhusu niingie mbinguni ili nile tunda la uzima?” Ni lazima ujue aina ya watu ambao Ninataka; wale walio najisi hawakubaliki kuingia katika ufalme, wale walio najisi hawakubaliki kuchafua nchi takatifu. Ingawa unaweza kuwa umefanya kazi nyingi, na umefanya kazi kwa miaka mingi, mwishowe kama bado wewe ni mwovu kupindukia—hakuvumiliki kwa sheria ya Mbinguni kwamba wewe unataka kuingia katika ufalme wangu! Tangu mwanzo wa dunia hadi leo, kamwe Sijatoa njia rahisi ya kuingilia ufalme Wangu kwa wale wenye neema Yangu. Hii ni sheria ya Mbinguni, na hakuna awezaye kuivunja. Ni lazima utafute uzima. Leo, wale watakaofanywa wakamilifu ni wa aina sawa na Petro: ni wale ambao hutafuta mabadiliko katika tabia yao wenyewe, na wako tayari kuwa na ushuhuda kwa Mungu na kutekeleza wajibu wao kama kiumbe wa Mungu. Ni watu kama hawa pekee watakaofanywa wakamilifu. Kama wewe tu unatazamia tuzo, na hutafuti kubadilisha tabia ya maisha yako mwenyewe, basi juhudi zako zote zitakuwa za bure—na huu ni ukweli usiobadilika!

Kutoka kwa tofauti katika kiini cha Paulo na kiini cha Petro unapaswa kufahamu kuwa wale wote ambao hawafuati uzima wanafanya kazi ya bure! Unamwamini Mungu na unafuata Mungu, na kwa hivyo moyoni mwako ni lazima umpende Mungu. Ni lazima uache tabia yako potovu, lazima utafute kutimiza mapenzi ya Mungu, na ni lazima utekeleze wajibu wako kama kiumbe wa Mungu. Kwa kuwa unamwamini na kumfuata Mungu, unapaswa kutoa kila kitu kwake, na hupaswi kufanya uamuzi au madai ya kibinafsi, na unapaswa kutimiza ukamilishaji wa mapenzi ya Mungu. Kwa kuwa uliumbwa, unapaswa kumtii Bwana aliyekuumba, kwa kuwa wewe huna mamlaka kiasili juu yako mwenyewe, na huna uwezo wa kudhibiti hatima yako. Kwa kuwa wewe ni mtu ambaye anamwamini Mungu, inapaswa utafute utakatifu na mabadiliko. Kwa kuwa wewe ni kiumbe wa Mungu, unapaswa kushika wajibu wako, na kuhifadhi nafasi yako, na ni lazima usivuke mpaka wa wajibu wako. Hii si kwa ajili ya kukuzuia, ama kukukandamiza kupitia mafundisho, bali ndiyo njia ambayo utaweza kutekelezea wajibu wako, na inaweza

kufikiwa—na inapaswa kufikiwa—na wote wanaotenda haki. Ukilinganisha kiini cha Petro na kiini cha Paulo, basi utajua jinsi unapaswa kutafuta. Kati ya njia ambazo Petro na Paulo walitembea, njia moja ni ya kufanywa mkamilifu, na nyingine ni njia ya kutolewa katika mashindano; Petro na Paulo wanawakilisha njia mbili tofauti. Ingawa kila moja wao alipokea kazi ya Roho Mtakatifu, na kila mmoja alipata nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu, na kila mmoja alikubali kile alichokuwa ameaminiwa na Bwana Yesu, tunda lililozaliwa katika kila mmoja wao halikuwa sawa. Mmoja kwa kweli alizaa tunda, na mwingine hukuzaa tunda. Kutokana na kiini cha kila mmoja wao, kazi waliyofanya, hiyo walioonyesha kwa upande wa nje, na hatima yao ya mwisho, unapaswa kuelewa ni njia gani unayopaswa kuchukua, njia ambayo unapaswa kuchagua kuitembea. Walitembelea njia mbili ambazo dhahiri ni tofauti. Paulo na Petro, walikuwa mifano ya kila njia, na kwa hivyo tangu mwanzo walionekana kuwakilisha njia hizi mbili. Je, ni mawazo gani muhimu katika uzoefu wa Paulo, na ni kwa nini yeye hakufaulu? Je, ni pointi gani muhimu katika matukio ya Petro, na ni jinsi gani yeye alishuhudia kufanywa mkalifu? Ukilinganisha kile ambacho kila alijali kuhusu, basi utajua aina hasa ya mtu ambaye Mungu anamtaka, mapenzi ya Mungu ni gani, na tabia ya Mungu, ni mtu wa aina gani ambaye hatimaye atafanywa mkamilifu, na pia aina gani ya mtu hawezi kufanywa mkamilifu, nini tabia ya wale ambao watafanywa wakamilifu, na nini tabia ya wale ambao hawatafanywa wakamilifu—masuala haya ya kiini yanaweza kuonekana katika uzoefu wa Petro na Paulo. Mungu aliumba kila kitu, na hivyo yeye hufanya viumbe wote kuwa chini ya utawala wake, na kujiwasilisha kwenye utawala wake; Yeye ataamuru kila kitu, ili kila kitu kiwe mikononi mwake. Vitu vyote vilivyoumbwa na Mungu, pamoja na wanyama, mimea, mwanadamu, milima na mito, na maziwa—vyote ni lazima vije chini ya utawala Wake. Vitu vyote mbinguni na ardhini lazima zije chini ya utawala Wake. Haviwezi kuwa na hiari yoyote na vyote ni lazima vitii mipango Yake. Hii iliagizwa na Mungu, na ni mamlaka ya Mungu. Mungu huamuru kila kitu, na huagiza na kuainisha kila kitu, ambapo kila kimoja huainishwa kulingana na aina, na kutengewa nafasi zao zenyewe, kulingana na mapenzi ya Mungu. Bila kujali kitu ni kikubwa namna gani, hakuna kitu kinachoweza kumpita Mungu, na vitu vyote ambavyo vinamtumikia mwanadamu aliyeumbwa na Mungu, na hakuna kitu kinachothubutu kumuasi Mungu ama kumdai Mungu. Na kwa hivyo mwanadamu, kama kiumbe wa Mungu, ni lazima atelezelele wajibu wa mwanadamu. Bila kujali iwapo yeye ni bwana au mlindaji wa vitu vyote, bila kujali jinsi hadhi ya mwanadamu ni kuu miongoni mwa vitu vyote, bado yeye ni binadamu mdogo anayetawaliwa na Mungu, na si zaidi ya binadamu asiye na umuhimu, kiumbe wa Mungu, na kamwe hatawahi kuwa juu ya Mungu. Kama kiumbe wa Mungu, mwanadamu anapaswa kutafuta kutekeleza wajibu wa kiumbe wa Mungu, na kutafuta kumpenda Mungu bila kufanya chaguo lingine kwa kuwa Mungu anastahiki upendo wa mwanadamu. Wale ambao wanatafuta kumpenda Mungu hawapaswi kutafuta faida zozote za kibinafsi au lile ambalo

wanatamani binafsi; hii ndiyo njia sahihi kabisa ya ufuatiliaji. Kama kile ambacho unatafuta ni ukweli, kile ambacho unatenda ni ukweli, na kile ambacho unafikia ni badiliko katika tabia yako, basi njia unayopitia ni sahihi. Iwapo utafutacho ni baraka za mwili, na kile unachoweka katika vitendo ni ukweli wa dhana zako mwenyewe, na iwapo hakuna mabadiliko katika tabia yako, na wewe si mtiifu kabisa kwa Mungu katika mwili, na bado unaishi kwenye mashaka, basi unachotafuta bila shaka kitakupeleka kuzimu, kwa kuwa njia ambayo unatembea ni njia ya kushindwa. Iwapo utafanywa mkamilifu ama utatolewa katika mashindano inategemea na harakati yako mwenyewe, ambayo pia ni kusema kuwa mafanikio au kushindwa kunategemea njia ambayo mwanadamu anapitia.

Kazi ya Mungu na Kazi ya Mwanadamu

Kiasi gani cha kazi ya mwanadamu ni kazi ya Roho Mtakatifu na uzoefu wa mwanadamu ni kiasi gani? Hata sasa, tunaweza kusema kuwa watu bado hawayaelewi maswali haya, ambayo yote ni kwa sababu watu hawayaelewi kanuni za utendaji kazi wa Roho Mtakatifu. Kazi ya mwanadamu Ninayoizungumzia, bila shaka, ikirejelea kazi za wale ambao wana kazi ya Roho Mtakatifu au wale ambao wanatumiwa na Roho Mtakatifu. Sizungumzii kazi ambayo inatokana na matakwa ya mwanadamu bali kazi ya mitume, watendaji kazi au ndugu wa kawaida waliopo katika mawanda ya kazi ya Roho Mtakatifu. Hapa, kazi ya mwanadamu hairejelei kazi ya Mungu mwenye mwili bali kwa mawanda na kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu kwa watu. Ingawa kanuni hizi ni kanuni na mawanda ya kazi ya Roho Mtakatifu, hazifanani na kanuni na mawanda ya kazi ya Mungu mwenye mwili. Kazi ya mwanadamu ina kiini na kanuni za mwanadamu, na kazi ya Mungu ina kiini na kanuni za Mungu.

Kazi katika mkondo wa Roho Mtakatifu, bila kujali ni kazi ya Mungu mwenyewe au ni kazi ya watu wanaotumiwa, ni kazi ya Roho Mtakatifu. Kiini cha Mungu Mwenyewe ni Roho, ambaye anaweza kuitwa Roho Mtakatifu au Roho mwenye nguvu mara saba. Kwa jumla, Wao ni Roho wa Mungu. Ni kwamba tu Roho wa Mungu anaitwa majina tofauti katika enzi tofauti tofauti. Lakini kiini Chao bado ni kimoja. Hivyo, kazi ya Mungu Mwenyewe ni kazi ya Roho Mtakatifu; kazi za Mungu mwenye mwili hazitofautiani na kazi za Roho Mtakatifu. Kazi ya wanadamu wanaotumiwa pia ni kazi ya Roho Mtakatifu. Ni kwamba tu kazi ya Mungu ni onyesho kamili la Roho Mtakatifu, ambalo ni ukweli kabisa, ilhali kazi ya watu wanaotumiwa inachanganyika na mambo mengi ya kibinadamu, na wala si uonyeshaji wa moja kwa moja wa Roho Mtakatifu, wala uonyeshaji kamili. Kazi ya Roho Mtakatifu ina mawanda mapana na wala haizuiliwi na hali yoyote ile. Kazi hiyo inatofautiana kwa watu tofauti tofauti, na kutoa viini tofauti tofauti vya kufanya kazi. Kazi pia inatofautiana katika enzi mbali mbali, kama pia ilivyo kazi tofauti katika nchi mbalimbali. Bila shaka, ingawa Roho Mtakatifu hufanya kazi katika njia

nyingi tofauti tofauti na kulingana na kanuni nyingi, haijalishi kazi imefanyikaje au kwa watu wa aina gani, kiini ni tofauti daima, na kazi Anazofanya kwa watu tofauti zote zina kanuni na zote zinaweza kuwakilisha kiini cha mhusika anayefanyiwa kazi. Hii ni kwa sababu kazi ya Roho Mtakatifu ni mahususi kabisa kwa mapana yake na inapimika. Kazi inayofanywa katika mwili uliopatikana si sawa na kazi inayofanywa kwa watu, na kazi hii pia inatofautiana kulingana na ubora mbali mbali wa tabia za watu. Kazi inayofanywa katika mwili uliopatikana si sawa na kazi inayofanywa kwa watu, na katika mwili uliopatikana Hafanyi kazi ile ile kama aliyoifanya kwa watu. Kwa ufupi, haijalishi Anafanya kazi jinsi gani, kazi katika vitu mbalimbali haifanani, na kanuni ambazo Anazitumia kufanya kazi zinatofautiana kulingana na hali na asili ya watu mbalimbali. Roho Mtakatifu anafanya kazi kwa watu tofauti tofauti kulingana na kiini chao cha asili na haweki mahitaji ambayo ni zaidi ya kiini chao cha asili, na wala Hafanyi kazi zaidi ya ubora halisi wa tabia yao. Kwa hivyo, kazi ya Roho Mtakatifu kwa mwanadamu inawaruhusu watu kuona kiini cha lengo la kazi hiyo. Kiini asili cha mwanadamu hakibadiliki; ubora halisi wa tabia ya mwanadamu ina mipaka. Kama Roho Mtakatifu anawatumia watu au anafanya kazi kwa watu kazi, kazi hiyo siku zote inafanywa kulingana na tabia za watu ili waweze kunufaika kutoka kwayo. Roho Mtakatifu anapofanya kazi kwa wanadamu wanaotumiwa, karama zao na tabia zao halisi zinatumiwa pia na wala haziachwi. Tabia zao halisi zinatumiwa zote kwa ajili ya kutoa huduma kwa kazi. Tunaweza kusema kuwa Anafanya kazi kwa kutumia sehemu zilizopo za wanadamu ili kupata matokeo yatendayo kazi. Kinyume chake, kazi inayofanyika katika mwili uliopatikana ni yenye kumwonyesha Roho moja kwa moja na wala haichanganywi na akili na mawazo ya mwanadamu, haifikiwi na karama za mwanadamu, uzoefu wa mwanadamu au hali ya ndani ya mwanadamu. Kazi nyingi mno ya Roho Mtakatifu yote inalenga kumnufaisha na kumwadilisha mwanadamu. Lakini baadhi ya watu wanaweza kukamilishwa wakati wengine hawana vigezo vya kuweza kukamilishwa, ambayo ni kusema, hawawezi kukamilishwa na ni vigumu sana kuokolewa, na ingawa wanaweza kuwa walishakuwa na kazi ya Roho Mtakatifu, mwishowe wanaondolewa. Hii ni sawa na kusema kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ni kuwaadilisha watu, hii haimaanishi kwamba wale wote waliokwisha kuwa na kazi ya Roho Mtakatifu wanapaswa kukamilishwa kikamilifu, kwa sababu njia wanayoifuatilia watu wengi si njia ya kukamilishwa. Wana kazi moja tu ya Roho Mtakatifu, na wala si ushirikiano wa kibinafsi wa binadamu au njia sahihi za kibinadamu. Kwa njia hii, kazi ya Roho Mtakatifu kwa watu hawa inakuwa kazi katika huduma ya wale ambao wanakamilishwa. Kazi ya Roho Mtakatifu haiwezi kuonwa moja kwa moja na watu au kuguswa moja kwa moja na watu wenyewe. Inaweza kuonyeshwa tu kwa njia ya msaada wa watu wenye karama ya kufanya kazi, ikiwa na maana kwamba kazi ya Roho Mtakatifu inatolewa kwa wafuasi kwa njia ya onyemaonyesho wanadamu.

Kazi ya Roho Mtakatifu inakamilishwa na kukamilika kupitia watu wa aina nyingi na hali

nyingi tofauti tofauti. Ingawa kazi ya Mungu mwenye mwili inaweza kuwakilisha kazi ya enzi zote, na inaweza kuwakilisha uingiaji wa watu katika enzi nzima, kazi kwa watu wengi bado inahitajika kufanywa na wanadamu wanaotumiwa na Roho Mtakatifu na sio na Mungu mwenye mwili. Kwa hivyo, kazi ya Mungu, au huduma ya Mungu mwenyewe, ni kazi ya Mungu mwenye mwili na haiwezi kufanywa na mwanadamu kwa niaba Yake. Kazi ya Roho Mtakatifu imekamilishwa kupitia watu wa aina mbalimbali na haiwezi kukamilishwa na mtu mahususi mmoja tu, au kufafanuliwa kikamilifu kupitia mtu mmoja mahususi. Wale ambao wanaongoza kanisa pia hawawezi kuiwakilisha kazi ya Roho Mtakatifu kikamilifu; wanaweza kufanya tu kazi fulani ya kuongoza. Kwa njia hii, kazi ya Roho Mtakatifu inaweza kugawanywa katika sehemu tatu: Kazi ya Mungu mwenyewe, kazi ya wanadamu wanaotumiwa, na kazi kwa wale wote walioko katika mkondo wa Roho Mtakatifu. Miongoni mwa hizo tatu, kazi ya Mungu ni kuongoza enzi nzima; kazi ya wanadamu wanaotumiwa ni kuwaongoza wafuasi wote wa Mungu kwa kutumwa au kupokea maagizo kwa ajili ya kazi ya Mungu mwenyewe; na wanadamu hawa ndio wanaoshirikiana na kazi ya Mungu; kazi inayofanywa na Roho Mtakatifu kwa wale waliopo katika mkondo wake ni kudumisha kazi Yake yote, yaani, kudumisha usimamizi wote na kudumisha ushuhuda Wake, na wakati uo huo kuwakamilisha wale wanaoweza kukamilishwa. Sehemu hizi tatu ni kazi kamili ya Roho Mtakatifu, lakini bila kazi ya Mungu Mwenyewe, kazi yote ya usimamizi inaweza kutuama. Kazi ya Mungu Mwenyewe inahusisha kazi ya wanadamu wote, na pia inawakilisha kazi ya enzi nzima. Hii ni kusema kwamba, kazi ya Mungu mwenyewe inawakilisha harakati na mwelekeo wa kazi yote ya Roho Mtakatifu, ilhali kazi ya mitume inafuata kazi ya Mungu na wala haiongozi enzi, na wala haiwakilishi mitindo ya kazi ya Roho Mtakatifu katika enzi nzima. Huwa wanafanya tu kazi ambayo mwanadamu anapaswa kufanya, ambayo haihusishi kabisa kazi ya usimamizi. Kazi ya Mungu ni mradi ndani ya kazi ya usimamizi. Kazi ya mwanadamu ni wajibu tu wa wanadamu kuweza kutumika na wala haina uhusiano na kazi ya usimamizi. Kwa sababu ya utambulisho na uwakilishaji tofauti wa kazi hii, licha ya ukweli kwamba zote ni kazi za Roho Mtakatifu, kuna tofauti za wazi na bainifu kati ya kazi ya Mungu na kazi ya mwanadamu. Aidha, kiwango cha kazi inayofanywa na Roho Mtakatifu kwa watu wenye tambulisho tofauti inatofautiana. Hizi ni kanuni na mawanda ya kazi ya Roho Mtakatifu.

Kazi ya mwanadamu inawakilisha uzoefu wake na ubinadamu wake. Kile ambacho mwanadamu anatoa na kazi ambayo anafanya vinamwakilisha yeye. Kuona kwa mwanadamu, kufikiri kwa mwanadamu, mantiki ya mwanadamu na uwezo wake mkubwa wa kufikiri vyote vinajumuishwa katika kazi yake. Kimsingi, uzoefu wa mwanadamu, unaweza zaidi kuwakilisha kazi yake na kile ambacho mtu amekipitia kitakuwa ni sehemu ya kazi yake. Kazi ya mwanadamu inaweza kuonyesha uzoefu wake. Pale ambapo baadhi ya watu wanapitia hali ya

kukaa tu bila kujishughulisha, sehemu kubwa ya ushirika wao inakuwa na vipengele vya uhasi. Kama uzoefu wao kwa kipindi cha muda ni mzuri na wanapita katika njia ya upande mzuri, kile wanachoshiriki kinatia moyo sana, na watu wanaweza kupokea mambo mazuri kutoka kwao. Mfanyakazi akiwa katika hali ya kukaa tu kwa kipindi cha muda, ushirika wake siku zote utakuwa na vipengele vya uhasi. Ushirika wa aina hii ni wa kuvunja moyo, na wengine watafunjika mioyo bila kujua kwa kufuata ushirika wa yule mfanyakazi. Hali ya wafuasi inabadilika kutegemea na hali ya kiongozi. Vile ambavyo mfanyakazi alivyo ndani, ndicho kile anachoonyesha, na kazi ya Roho Mtakatifu mara nyingi inabadilika kulingana na hali ya mwanadamu. Anafanya kazi kulingana na uzoefu wa mwanadamu na wala hamshurutishi mwanadamu bali anamsihi mwanadamu kulingana na hali yake ya kawaida ya uzoefu wake. Hii ni kusema kwamba ushirika wa mwanadamu unatofautiana na neno la Mungu. Kile ambacho mwanadamu hushiriki kinaeleza vile anavyotazama mambo na uzoefu wake, kinaonyesha kile wanachokiona na kupitia uzoefu kwa msingi wa kazi ya Mungu. Wajibu wao ni kutafuta, baada ya Mungu kufanya kazi au kuzungumza, kile wanachopaswa kufanya au kuingia kwacho, halafu kukiwasilisha kwa wafuasi. Hivyo, kazi ya mwanadamu inawakilisha kuingia au matendo yake. Bila shaka, kazi hiyo imechanganyika na masomo ya kibinadamu na uzoefu au mawazo ya kibinadamu. Haijalishi namna ambavyo Roho Mtakatifu anafanya kazi, ama Anavyomfanyia kazi mwanadamu au Mungu mwenye mwili, siku zote watenda kazi ndio wanaoonyesha vile walivyo. Ingawa ni Roho Mtakatifu ambaye hufanya kazi, kazi hiyo imejengwa katika msingi wa mwanadamu alivyo kiasili, kwa sababu Roho Mtakatifu hafanyi kazi pasipo msingi. Kwa maneno mengine, kazi haifanyiki pasipokuwa na kitu, lakini siku zote hufanyika kulingana na mazingira halisi na hali halisi. Ni kwa njia hii pekee ndiyo tabia ya mwanadamu inaweza kubadilishwa, kwamba mitazamo yake ya zamani na mawazo yake ya zamani yanaweza kubadilishwa. Kile ambacho mwanadamu huonyesha ni kile anachokiona, kupitia uzoefu na kukitafakari. Hata kama ni mafundisho au fikira, haya yote hufikiwa na fikira za mwanadamu. Bila kujali ukubwa wa kazi ya mwanadamu, haiwezi kuzidi mawanda ya uzoefu wa mwanadamu, kile ambacho mwanadamu huona, au kile ambacho mwanadamu anaweza kukitafakari au kuingia akilini mwake. Kile ambacho Mungu anaonyesha ndivyo hivyo Mungu Mwenyewe alivyo, na hii ni nje ya uwezo wa mwanadamu, yaani, nje ya uwezo wa kufikiri kwa mwanadamu. Anaonyesha kazi Yake ya kuwaongoza wanadamu wote, na hii haihusiani na undani wa uzoefu wa mwanadamu, badala yake inahusu usimamizi Wake. Mwanadamu anaonyesha uzoefu wake wakati Mungu anaonyesha nafsi Yake—nafsi hii ni tabia Yake ya asili na iko nje ya uwezo wa mwanadamu. Uzoefu wa mwanadamu ni kuona kwake na kupata maarifa kulingana na uonyeshaji wa Mungu wa nafsi Yake. Kuona kama huko na maarifa kama hayo yanaitwa asili ya mwanadamu. Yanaonyeshwa kwa msingi wa tabia asili ya mwanadamu na ubora wa tabia yake halisi; hivyo pia vinaitwa nafsi ya mwanadamu. Mwanadamu anaweza

kushiriki kile anachokipitia na kukiona. Kile ambacho hujawahi kukipitia au kukiona au akili yake haiwezi kukifikia, yaani, vitu ambavyo havipo ndani yake, hawezi kuvishiriki. Ikiwa kile ambacho mwanadamu anakionyesha sio uzoefu wake, basi ni mawazo yake au mafundisho ya kidini. Kwa ufupi, hakuna ukweli wowote katika maneno yake. Kama hujawahi kukutana na maswala ya jamii, hutaweza kushiriki kwa uwazi kwenye mahusiano changamani katika jamii. Kama huna familia na watu wengine wanazungumza juu ya masuala ya familia, huwezi kuelewa kiasi kikubwa cha kile walichokuwa wakisema. Kwa hivyo, kile ambacho mwanadamu anakifanyia ushirika na kazi anayofanya vinawakilisha asili yake ya ndani. Ikiwa mtu anafanya ushirika kuhusu ufahamu wake wa kuadibu na hukumu, lakini huna uzoefu wake, usithubutu kukana maarifa yake, badala yake kuwa na uhakika wa anachokisema kwa asilimia mia moja. Hii ni kwa sababu kile anachokifanyia ushirika ni kitu ambacho hujawahi kupata uzoefu wake, kitu ambacho hujawahi kukifahamu, na akili yako haiwezi kukitafakari. Unaweza tu kujifunza kutoka kwa ufahamu wake njia za maisha yajayo yanayohusiana na kuadibu na hukumu. Lakini njia hii inaweza kufanya kazi tu kama ufahamu uliojikita katika fundisho na haiwezi kuchukua nafasi ya ufahamu wako, na zaidi sana uzoefu wako. Pengine unafikiri kwamba kile anachokisema ni sahihi, lakini unapokipitia, unagundua kwamba hakitekelezeki katika mambo mengi. Pengine unahisi kwamba maarifa fulani unayoyasikia hayatekelezeki kabisa; unakuwa na mtazamo kuhusu maarifa hayo kwa wakati fulani, na ingawa unayakubali, unafanya hivyo shingo upande. Lakini unapopata uzoefu, maarifa yanayokupa mtazamo ndiyo yanayoongoza matendo yako. Na kadiri unavyotenda, ndivyo unavyozidi kuelewa thamani halisi na maana ya maneno yake. Baada ya kuwa na uzoefu, sasa unaweza kuzungumza juu ya maarifa unayopaswa kuwa nayo kuhusu vitu ulivyovipitia. Aidha, unaweza pia kutofautisha kati ya wale ambao maarifa yao ni halisi na ya utendaji na wale ambao maarifa yao yamejikita katika mafundisho ya kidini na hayana thamani. Kwa hivyo, kama maarifa ambayo unayazungumzia yanapatana na ukweli kwa kiasi kikubwa yanategemea na iwapo una uzoefu wa vitendo. Pale palipo na ukweli katika uzoefu wako, maarifa yako yatakuwa yanatekelezeka na yenye thamani. Kupitia uzoefu wako, pia unaweza kupata utambuzi na umaizi, kukuza maarifa yako, na kuongeza hekima yako na akili ya kuzaliwa katika kujiongoza. Maarifa yanayozungumzwa na watu ambao hawana ukweli ni fundisho la kidini tu, bila kujali yana nguvu kiasi gani. Mtu wa aina hii anaweza kuwa mwenye akili sana yanapokuja masuala ya kimwili lakini hawezi kutofautisha yanapokuja masuala ya kiroho. Hii ni kwa sababu watu kama hao hawana uzoefu wowote katika masuala ya kiroho. Hawa ni watu ambao hawajapata nuru katika masuala ya kiroho na hawaelewi mambo ya kiroho. Haijalishi aina ya maarifa unayoonyesha, ilimradi ni asili yako, basi ni uzoefu wako binafsi, maarifa yako halisi. Kile ambacho watu wenye mafundisho tu huzungumzia, yaani, wale ambao hawana ukweli au uhalisi, huzungumzia yaweza kusemwa kuwa ni asili yao, kwa sababu mafundisho yao yamefikwa kwa njia ya kutafakari sana na ni matokeo ya akili yao kutafakari

kwa kina, lakini ni mafundisho tu, si kitu chochote zaidi ya fikira. Uzoefu wa aina tofauti za watu unawakilisha vitu vilivyomo ndani yao. Wale wote ambao hawana uzoefu wa kiroho hawawezi kuzungumza juu ya maarifa ya ukweli, maarifa sahihi kuhusu aina mbalimbali za masuala ya kiroho. Kile ambacho mtu anakionyesha ndivyo alivyo ndani—hili ni hakika. Ikiwa mtu anatamani kuwa na maarifa ya masuala ya kiroho na ukweli, anapaswa kuwa na uzoefu halisi. Ikiwa huwezi kuzungumza wazi juu ya masuala ya kawaida yanayohusiana na maisha ya mwanadamu, basi utawezaje kuzungumzia masuala ya kiroho? Wale wanaoweza kuyaongoza makanisa, kuwaruzuku watu maisha, na kuwa mtume kwa watu, wanapaswa kuwa na uzoefu halisi, ufahamu sahihi wa masuala ya kiroho, kuelewa vyema na kuwa na uzoefu wa ukweli. Watu wa namna hiyo tu ndio wanaostahili kuwa watenda kazi au mitume wanaoyaongoza makanisa. Vinginevyo, wanaweza kutufuata tu kidogo na hawawezi kuongoza, sembuse kuwa mtume mwenye uwezo wa kuwapatia watu uhai. Hii ni kwa sababu kazi ya mitume siyo kukimbia au kupigana; ni kufanya kazi ya kutoa huduma ya maisha na kuwaongoza wengine katika kubadili tabia zao. Wale wanaofanya kazi hii wanaagizwa kubeba mzigo mkubwa, ambao si kitu ambacho kila mtu anaweza kufanya. Kazi ya aina hii inaweza tu kufanywa na wale ambao wana maisha ya uwepo, yaani, wale ambao wana uzoefu wa ukweli. Haiwezi kufanywa na kila mtu ambaye anaweza kukata tamaa, anaweza kukimbia au yupo tayari kutumia pesa; watu ambao hawana uzoefu wa ukweli, wale ambao hawajapogolewa au kuhukumikiwa, hawawezi kufanya kazi ya aina hii. Watu ambao hawana uzoefu, yaani, watu wasio na ukweli, hawawezi kuona ukweli kwa uwazi kwa kuwa wao wenyewe hawako katika hali hii. Hivyo, mtu wa aina hii si kwamba hawezi tu kufanya kazi ya kuongoza bali atakuwa mlengwa wa kuondolewa ikiwa hatakuwa na ukweli kwa muda mrefu. Kuona unakokuzungumzia kunaweza kuthibitisha ugumu ulioupitia maishani, katika masuala ambayo kwayo umeadibiwa na katika mambo ambayo umehukumikiwa kwayo. Hii pia ni kweli katika majaribu: Vitu ambavyo mtu anasafishwa kwavyo, vitu ambavyo kwavyo mtu ni mdhaifu, hivi ni vitu ambavyo mtu ana uzoefu kwavyo, vitu ambavyo mtu anaelewa njia zake. Kwa mfano, kama mtu amekatishwa tamaa katika ndoa, muda mwingi atakuwa anafanya ushirika, “Asante Mungu, msifu Mungu, ni lazima nitimize matakwa ya Mungu, na kuyatoa maisha yangu yote, kuikabidhi ndoa yangu kikamilifu katika mikono ya Mungu. Niko radhi kuyatoa maisha yangu yote kwa Mungu.” Vitu vyote ndani ya mwanadamu vinaweza kuonyesha kile alichokupitia katika ushirika. Mwendo wa usemi wa mtu, kama anazungumza kwa sauti kubwa au kwa sauti ya chini, masuala kama hayo ambayo si masuala ya uzoefu hayawezi kuwakilisha kile alichokacho na kile alichokacho. Yanaweza kueleza tu iwapo tabia yake ni nzuri au mbaya, au kama asili yake ni nzuri au mbaya lakini haiwezi kulinganishwa na kama ana uzoefu. Uwezo wa mtu kujionyesha anapozungumza, ama ujuzi au kasi ya kuzungumza, ni suala tu la utendaji na haliwezi kuchukua nafasi ya uzoefu wake. Unapozungumza juu ya uzoefu wako binafsi, unafanya ushirika wa kile ambacho unakipatia

umuhimu na vitu vyote ndani yako. Usemi Wangu unawakilisha asili Yangu, lakini kile Ninachokisema kiko nje ya uwezo wa mwanadamu. Kile Nikisemacho sio kile ambacho mwanadamu anakipitia, na sio kitu ambacho mwanadamu anaweza kukiona, pia si kitu ambacho mwanadamu anaweza kukigusa, lakini ndicho Nilicho. Baadhi ya watu wanakiri tu kwamba kile Ninachokifanyia ushirika ndicho kile Nimekipitia, lakini hawatambui kwamba ni maonyesho ya moja kwa moja ya Roho. Ni kweli, kile Ninachokisema ndicho kile Nimekipitia. Ni Mimi Ndiye Niliyefanya kazi ya usimamizi kwa kipindi cha zaidi ya miaka elfu sita. Nimepitia kila kitu kuanzia mwanzo wa uumbaji wa mwanadamu hadi leo; Nitashindwaje kukizungumzia? Linapokuja suala la asili ya mwanadamu, Nimeliona waziwazi, na Nimeliangalia toka zamani; sasa Nitashindwaje kuliongelea? Kwa kuwa nimeiona asili ya mwanadamu kwa uwazi, Nina sifa za kumrudi mwanadamu na kumhukumu, kwa sababu mwanadamu mzima ametoka Kwangu lakini ameharibiwa na Shetani. Kwa ukweli, Nimehitimu kutathmini kazi ambayo Nimeifanya. Ingawa kazi hii haijafanywa na mwili Wangu, ni uonyeshaji wa moja kwa moja wa Roho, na hiki ndicho Nilicho nacho na kile Nilicho. Kwa hivyo, Ninaweza kuonyesha na kufanya kazi ambayo Napaswa kufanya. Kile ambacho mwanadamu anakisema ni kile alichokipitia. Ni kile ambacho wamekiona, kile ambacho akili zao zinaweza kukifikia, na kile ambacho milango yao ya fahamu inaweza kuhisi. Hicho ndicho wanachoweza kukifanyia ushirika. Maneno yaliyosemwa na mwili wa Mungu ni onyesho la moja kwa moja la Roho na huonyesha kazi ambayo imefanywa na Roho. Mwili haujaipitia au kuiona, lakini bado huonyesha asili Yake kwa sababu kiini cha mwili ni Roho, na huonyesha kazi ya Roho. Ingawa mwili hauwezi kuifikia, ni kazi ambayo tayari imefanywa na Roho. Baada ya kufanyika mwili, kupitia uonyeshaji wa mwili, Anawasaidia watu kujua asili ya Mungu na kuwafanya watu kuiona tabia ya Mungu na kazi ambayo Ameifanya. Kazi ya mwanadamu inawawezesha watu kuelewa kwa uwazi kuhusu kile wanachopaswa kuingia kwacho na wanachopaswa kuelewa; inahusisha kuwaongoza watu kupata ufahamu na kuujua ukweli. Kazi ya mwanadamu ni kuwaendeleza watu; kazi ya Mungu ni kufungua njia mpya na kufungua enzi mpya kwa ajili ya binadamu, na kuwafunulia watu kile ambacho hakijafahamika kwa watu wenye mwili wa kufa, ikiwasaidia kuelewa tabia Yake. Kazi ya Mungu ni kuwaongoza wanadamu wote.

Kazi ya Roho Mtakatifu ni kuhusu kuwasaidia watu kupata faida; ni kuwaadilisha watu; hakuna kazi ambayo haiwanufaishi watu. Haijalishi kama ukweli ni wa kina au usio wa kina, na haijalishi tabia ya wale wanaopokea ukweli huo ilivyo, chochote ambacho Roho Mtakatifu anafanya, yote hayo huwanufaisha watu. Lakini kazi ya Roho Mtakatifu haiwezi kufanywa moja kwa moja; ni lazima ifanywe na wanadamu wanaoshirikiana na Yeye. Ni kwa njia hii pekee ndiyo matokeo ya kazi ya Roho Mtakatifu yanaweza kupatikana. Bila shaka, inapokuwa ni kazi ya moja kwa moja ya Roho Mtakatifu, haijachanganywa na kitu chochote kabisa; lakini

inapotumia mwanadamu kama chombo, inakuwa imechanganywa sana na sio kazi halisi ya Roho Mtakatifu. Kwa njia hii, ukweli hubadilika katika viwango tofauti. Wafuasi hawapokei nia halisi ya Roho Mtakatifu bali wanapokea muungano wa kazi ya Roho Mtakatifu na uzoefu na maarifa ya mwanadamu. Sehemu ya kazi ya Roho Mtakatifu inayopokelewa na wafuasi ni sahihi. Uzoefu na maarifa ya mwanadamu yanayopokewa yanatofautiana kwa sababu watenda kazi ni tofauti. Watenda kazi wanapokuwa na nuru na uongozi wa Roho Mtakatifu, wanakuwa wanapata uzoefu kulingana na nuru na uongozi huu. Ndani ya uzoefu huu kuna akili ya mwanadamu na uzoefu, vile vile asili ya ubinadamu, ambapo wanapata maarifa na kuona vile walivyopaswa kuona. Hii ndiyo njia ya kutenda baada ya mwanadamu kuujuu ukweli. Namna hii ya kutenda siku zote haifanani kwa sababu watu wana uzoefu tofauti na vitu ambavyo watu wanavipitia ni tofauti. Kwa njia hii, nuru ile ile ya Roho Mtakatifu inaleta maarifa tofauti na desturi kwa sababu wale wanaopokea nuru hiyo ni tofauti. Baadhi ya watu hufanya makosa madogo wakati wa utendaji ilhali wengine hufanya makosa makubwa, na baadhi hawafanyi chochote ila ni makosa tu. Hii ni kwa sababu uwezo wa kuelewa mambo unatofautiana na kwa sababu tabia zao halisi pia zinatofautiana. Baadhi ya watu wanaelewa hivi baada ya kuusikia ujumbe, na baadhi ya watu wanauelewa vile baada ya kuusikia ukweli. Baadhi ya watu wanapotoka kidogo; na baadhi hawaelewi kabisa maana ya ukweli. Kwa hiyo, kwa jinsi yoyote mtu aelewavyo ndivyo atakavyowaongoza wengine; hii ni kweli kabisa, kwa sababu kazi yake inaonyesha asili yake tu. Watu wanaoongozwa na watu wenye ufahamu sahihi wa ukweli pia watakuwa na ufahamu sahihi wa ukweli. Hata kama kuna watu ambao uelewa wao una makosa, ni wachache sana, na sio watu wote watakuwa na makosa. Ikiwa mtu ana makosa katika anavyoelewa ukweli, wale wanaomfuata bila shaka pia watakuwa na makosa. Watu hawa watakuwa na makosa katika kila namna. Kiwango cha kuelewa ukweli miongoni mwa wafuasi kinategemea kwa kiasi kikubwa watenda kazi. Bila shaka, ukweli kutoka kwa Mungu ni sahihi na hauna makosa, na ni hakika. Lakini, watenda kazi hawako sahihi kikamilifu na hatuwezi kusema kwamba ni wa kutegemewa kabisa. Ikiwa watenda kazi wana njia ya kuuweka ukweli katika njia ya matendo, basi wafuasi pia watakuwa na njia ya kuutenda. Ikiwa watenda kazi hawawezi kuuweka ukweli katika matendo bali wanashikilia mafundisho tu, wafuasi hawatakuwa na uhalisia wowote. Ubora wa tabia na asili ya wafuasi vinaukiliwa na kuzaliwa na havihusiani na watenda kazi. Lakini kiwango ambacho kwacho wafuasi wanauelewa ukweli na kumfahamu Mungu kinategemeana na watenda kazi (hii ni kwa baadhi ya watu tu). Vyovyote alivyo mtenda kazi, hivyo ndivyo wafuasi anaowaongoza watakavyokuwa. Kile ambacho mtenda kazi anakionyesha ni asili yake mwenyewe, bila kuacha chochote. Yale anayowaambia wafuasi wake watende ndiyo yeye mwenyewe yuko radhi kuyafikia au ni yale anayoweza kutimiza. Watenda kazi wengi huwaambia wafuasi wao kufuata mambo fulani kulingana na yale wao wenyewe wanayoyafanya, licha ya kuwepo mengi ambayo watu hawawezi kuyafikia kabisa. Kile ambacho watu hawawezi

kufanikisha kinakuwa kizuizi katika kuingia kwao.

Kuna mkengeuko mdogo zaidi katika kazi ya wale ambao wamepitia kupogolewa, kushughulikiwa, hukumu na kuadibu, na uonyeshaji wa kazi zao ni sahihi zaidi. Wale wanaotegemea asili yao katika kufanya kazi wanafanya makosa makubwa sana. Kuna uasili mwingi sana katika kazi ya watu ambao si wakamilifu, kitu ambacho kinaweka kizuizi kikubwa katika kazi ya Roho Mtakatifu. Bila kujali jinsi ubora wa tabia ya mtu ulivyo mzuri, lazima pia apitie upogoaji, ashughulikiwe, na kuhukumiwa kabla aweze kufanya kazi ya agizo la Mungu. Kama hajapitia hukumu kama hiyo, kwa namna yoyote nzuri ile atakavyofanya, haiwezi kuambatana na kanuni za ukweli na ni uasili kabisa na uzuri wa mwanadamu. Kazi ya wale ambao wamepitia kupogolewa, kushughulikiwa, na hukumu ni sahihi zaidi kuliko kazi ya wale ambao hawajapogolewa, kushughulikiwa, na hukumiwa. Wale ambao hawajapitia hukumu hawaonyeshi chochote isipokuwa mawazo ya kibinadamu, yakiwa yamechanganyika na ufahamu wa kibinadamu na talanta za ndani. Sio maonyesho sahihi wa mwanadamu wa kazi ya Mungu. Watu wanaowafuata wanaletwa mbele yao kwa tabia yao ya ndani. Kwa sababu wanaonyesha vitu vingi vya kuona na uzoefu wa mwanadamu, ambavyo takribani havina muungano na nia ya asili ya Mungu, na hutofautiana sana nayo, kazi ya mtu wa aina hii haiwezi kuwaleta watu mbele ya Mungu, bali badala yake huwaleta mbele ya mwanadamu. Hivyo, wale ambao hawajapitia hukumu na kuadibu, hawana sifa za kufanya kazi ya agizo la Mungu. Kazi ya mtenda kazi mwenye sifa inaweza kuwaleta watu katika njia sahihi na kuwaruhusu kuzama kwa kina katika ukweli. Kazi anayofanya inaweza kuwaleta watu mbele ya Mungu. Aidha, kazi anayofanya inaweza kutofautiana kutoka kwa mtu hadi mtu mwingine na wala haifungwi na kanuni, inawapa watu uhuru. Aidha, wanaweza kukua katika uzima kwa taratibu, wakiendelea kukua na kuzama ndani kabisa katika ukweli. Kazi ya mtenda kazi asiye hitimu haifikii kiwango hiki; kazi yake ni ya kipumbavu. Anaweza kuwaleta watu katika kanuni tu; kile anachowataka watu kufanya hakitofautiani kati ya mtu na mtu mwingine; hafanyi kazi kulingana na mahitaji halisi ya watu. Katika kazi ya aina hii kunakuwa na kanuni nyingi sana na mafundisho mengi sana, na haiwezi kuwaleta watu katika uhalisia au katika hali ya kawaida ya kukua katika uzima. Inaweza kuwawezesha watu tu kusimama kwa kanuni chache zisizokuwa na maana. Uongozi wa namna hii unaweza tu kuwapotosha watu. Anakuongoza ili uwe kama yeye; anaweza kukuleta katika kile anacho na kile alicheo. Kwa wafuasi kutambua endapo viongozi wana sifa, jambo la muhimu ni kuangalia njia wanayoiongoza na matokeo ya kazi yao, na kuangalia iwapo wafuasi wanapokea kanuni kulingana na ukweli, na kama wanapokea namna ya kutenda kunakowafaa wao ili waweze kubadilishwa. Unapaswa kutofautisha kati ya kazi tofauti za aina tofauti za watu; haupaswi kuwa mfuasi mpumbavu. Hili linaathiri suala la kuingia kwako. Kama huwezi kutofautisha ni uongozi wa mtu yupi una njia na upi hauna, utadanganywa kwa urahisi. Haya

yote yana athari ya moja kwa moja katika maisha yako. Kuna mambo mengi ya asili katika kazi ya mtu ambaye hajakamilishwa; matakwa mengi ya kibinadamu yamechanganywa humo. Hali yao ni ya asili, kile walichozaliwa nacho, si maisha baada ya kupitia kushughulikiwa au uhalisia baada ya kubadilishwa. Ni kwa namna gani mtu wa aina hii ya mtu anaweza kuunga mkono utafutaji wa uzima? Maisha halisi ya mwanadamu ni akili au talanta yake ya ndani. Aina hii ya akili au talanta ni kinyume cha kile hasa ambacho Mungu anamtaka mwanadamu afanye. Ikiwa mwanadamu hajakamilishwa na tabia yake potovu haijapogolewa na kushughulikiwa, kutakuwa na pengo kubwa kati ya kile anachokionyesha na ukweli; utachanganywa na vitu visivyoeleweka vizuri kama vile tafakari zake na uzoefu wa upande mmoja, n.k. Aidha, bila kujali jinsi anavyofanya kazi, watu wanahisi kwamba hakuna lengo la jumla na hakuna ukweli ambao unafaa kwa kuingia watu wote. Matakwa mengi yanawekwa kwa watu wakitakiwa kufanya kile ambacho ni nje ya uwezo wao, kumwingiza bata katika kitulio cha ndege. Hii ni kazi ya matakwa ya binadamu. Tabia potovu ya mwanadamu, mawazo yake na fikira vinaenea katika sehemu zote za mwili wake. Mwanadamu hakuzaliwa na tabia ya kutenda ukweli, na wala hana tabia ya kuuelewa ukweli moja kwa moja. Ikiongezwa kwa upotovu ya mwanadamu—mtu wa aina hii ya asili anapofanya kazi, je, si yeye husababisha ukatizaji? Lakini mwanadamu ambaye amekamilishwa ana uzoefu wa ukweli ambao watu wanapaswa kuuelewa, na maarifa ya tabia yao potovu, ili kwamba vitu visivyoeleweka vizuri na visivyokuwa halisi katika kazi yake vididimie kwa taratibu, ughushi wa binadamu upungue, na kazi na huduma yake yakaribie zaidi viwango vinavyohitajika na Mungu. Hivyo, kazi yake imeingia katika uhalisi wa ukweli na pia imekuwa halisi zaidi. Mawazo katika akili ya mwanadamu yanazuia kazi ya Roho Mtakatifu. Mwanadamu ana fikira nzuri na mwenye mantiki ya maana na uzoefu mkongwe katika kukabiliana na mambo. Kama haya yote hayatapitia kupogolewa na kusahihishwa, yote yanakuwa vizuizi katika kazi. Hivyo kazi ya mwanadamu haiwezi kufikia kiwango cha juu cha usahihi, hususan kazi ya watu ambao hawajakamilishwa.

Kazi ya mwanadamu ina mipaka na kadiri inavyoweza kufika. Mtu mmoja anaweza tu kufanya kazi ya wakati fulani na hawezi kufanya kazi ya enzi nzima—vinginevyo, angewaongoza watu katika kanuni. Kazi ya mwanadamu inaweza kufaa tu katika kipindi au awamu fulani. Hii ni kwa sababu uzoefu wa mwanadamu una mawanda. Mtu hawezi kulinganisha kazi ya mwanadamu na kazi ya Mungu. Njia za mwanadamu kutenda na maarifa yake ya ukweli yote yanatumika tu katika mawanda fulani. Huwezi kusema kwamba njia ambayo mwanadamu anaiendea ni matakwa ya Roho Mtakatifu kabisa, kwa sababu mwanadamu anaweza kupewa nuru na Roho Mtakatifu tu na hawezi kujazwa kikamilifu na Roho Mtakatifu. Vitu ambavyo mwanadamu anaweza kuvipitia vyote vipo ndani ya mawanda ya ubinadamu na haviwezi kuzidi mawanda ya fikira katika akili ya kawaida ya mwanadamu. Wale wote

wanaoweza kuishi kwa kudhihirisha uhalisi wa ukweli hupitia ndani ya mawanda haya. Wanapoupitia ukweli, siku zote ni uzoefu wa maisha ya kawaida ya mwanadamu chini ya nuru ya Roho Mtakatifu, sio kupitia uzoefu kwa namna ambayo inakengeuka kutoka kwa maisha ya kawaida ya mwanadamu. Wanapitia uzoefu wa ukweli ambao unatiwa nuru na Roho Mtakatifu katika msingi wa kuishi maisha yao ya kibinadamu. Aidha, ukweli huu unatofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, na kina chake kinahusiana na hali ya mtu huyo. Mtu anaweza kusema kwamba njia anayoipitia ni maisha ya kawaida ya kibinadamu ya mwanadamu kufuatilia ukweli na kwamba hiyo ndiyo njia ambayo mtu wa kawaida ambaye amepata nuru ya Roho Mtakatifu anaipita. Huwezi kusema kwamba njia wanayoipitia ni njia ambayo inafuatwa na Roho Mtakatifu. Katika uzoefu wa kawaida wa binadamu, kwa sababu watu wanaoutafuta ukweli hawafanani, kazi ya Roho Mtakatifu pia haifanani. Aidha, kwa sababu mazingira wanayoyapitia na kiwango cha uzoefu wao havifanani, kwa sababu ya mchanganyiko wa akili na mawazo yao, uzoefu wao pia umechanganyika kwa kiwango tofauti. Kila mtu anaelewa ukweli kulingana na hali yake tofauti ya kibinafsi. Ufahamu wao wa maana halisi ya ukweli hauko kamili, na ni kipengele chake kimoja tu au vichache. Mawanda ambayo ukweli unaeleweka kwa mwanadamu siku zote umejikita katika hali tofauti tofauti za watu, na hivyo hazifanani. Kwa njia hii, maarifa yanayoonyesha ukweli ule ule na watu tofauti havifanani. Huu kusema, uzoefu wa mwanadamu siku zote una mipaka, na hauwezi kuwakilisha kikamilifu matakwa ya Roho Mtakatifu, na kazi ya mwanadamu haiwezi kuchukuliwa kama kazi ya Mungu, hata kama kile kinachoonyeshwa na mwanadamu kinafanana kwa karibu sana na mapenzi ya Mungu, hata kama uzoefu wa mwanadamu unakaribiana sana na kazi ya ukamilifu itakayofanywa na Roho Mtakatifu. Mwanadamu anaweza kuwa tu mtumishi wa Mungu, akifanya kazi ambayo Mungu amemwaminia. Mwanadamu anaweza kuonyesha maarifa tu chini ya nuru ya Roho Mtakatifu na ukweli alioupata kutokana na uzoefu wake binafsi. Mwanadamu hana sifa na hana vigezo vya kuwa njia ya Roho Mtakatifu. Hana uwezo wa kusema kuwa kazi ya mwanadamu ni kazi ya Mungu. Mwanadamu ana kanuni za kufanya kazi za mwanadamu, na wanadamu wote wana uzoefu tofauti na wana hali zinazotofautiana. Kazi ya mwanadamu inajumuisha uzoefu wake wote chini ya nuru ya Roho Mtakatifu. Uzoefu huu unaweza tu kuwakilisha asili ya mwanadamu na hauwakilishi asili ya Mungu, au mapenzi ya Roho Mtakatifu. Kwa hivyo, njia anayoipita mwanadamu haiwezi kusemwa kuwa njia anayoipita Roho Mtakatifu, kwa sababu kazi ya mwanadamu haiwezi kuwakilisha kazi ya Mungu na kazi ya mwanadamu na uzoefu wa mwanadamu sio matakwa ya Roho Mtakatifu. Kazi ya mwanadamu ina hatari ya kuangukia katika kanuni, na mbinu za kazi yake zimefinywa katika uelewa wake finyu na hawezi kuwaongoza watu katika njia huru. Wafuasi wengi wanaishi ndani ya mawanda finyu, na uzoefu wao pia unakuwa ni finyu. Uzoefu wa mwanadamu siku zote ni finyu; mbinu ya kazi yake pia ni finyu na haiwezi kulinganishwa na kazi ya Roho Mtakatifu au kazi ya Mungu Mwenyewe—hii

ni kwa sababu uzoefu wa mwanadamu, hatimaye, ni finyu. Hata hivyo Mungu anafanya kazi Yake, hakuna kanuni kwa kazi yake; vyovyote vile inavyofanywa, haifungwi na njia moja. Hakuna kanuni za aina yoyote ile katika kazi ya Mungu—kazi Yake yote ni huru na ni bure. Haijalishi ni muda kiasi gani mwanadamu anatumia kumfuata Yeye, hawawezi kutengeneza sheria zozote za njia anavyofanya kazi. Ingawaje kazi Yake inaongozwa na kanuni, siku zote inafanywa katika njia mpya na siku zote inakuwa na maendeleo mapya ambayo yanazidi uwezo wa mwanadamu. Katika kipindi fulani, Mungu anaweza kuwa na njia nyingi tofauti tofauti za kazi na njia tofauti za kuongoza, Akiruhusu watu siku zote kuwa na kuingia kupya na mabadiliko mapya. Huwezi kuelewa sheria za kazi Yake kwa sababu siku zote Anafanya kazi katika njia mpya. Ni kwa njia hii tu ndiyo wafuasi wa Mungu hawawezi kuanguka katika kanuni. Kazi ya Mungu Mwenyewe siku zote inaepuka mitazamo ya watu na kupinga mitazamo yao. Ni wale tu ambao wanamfuata Yeye kwa moyo wote ndio wanaoweza kubadilishwa tabia zao na wanaweza kuishi kwa uhuru bila kuwa chini ya kanuni zozote au kufungwa na mitazamo yoyote ya kidini. Madai ambayo kazi ya mwanadamu inawawekea watu yamejikita katika uzoefu wake mwenyewe na kile ambacho yeye mwenyewe anaweza kutimiza. Kiwango cha matakwa haya kimejifunga ndani ya mawanda fulani, na mbinu za kutenda pia ni finyu sana. Kwa hivyo wafuasi bila kutambua huishi ndani ya matakwa finyu; kadiri muda unavyokwenda, yanakuwa kanuni na taratibu za kidini. Ikiwa kazi ya kipindi fulani inaongozwa na mtu ambaye hajapitia kukamilishwa na Mungu na hakupokea hukumu, wafuasi wake wote watakuwa wadini na wataalamu wa kumpinga Mungu. Kwa hivyo, ikiwa mtu fulani ni kiongozi aliyehitimu, mtu huyo anapaswa kuwa amepitia hukumu na kukubali kukamilishwa. Wale ambao hawajapitia mchakato wa hukumu, hata kama wanaweza kuwa na kazi ya Roho Mtakatifu, wanaonyesha vitu ambavyo si dhahiri na visivyokuwa halisi. Kadiri muda unavyozidi kwenda, watawaongoza watu katika kanuni zisizoeleweka vizuri na za kimuujiza. Kazi ambayo Mungu anafanya haiambatani na mwili wa mwanadamu; haiambatani na mawazo ya mwanadamu bali inapinga mitazamo ya mwanadamu; haijachanganyika na mitazamo ya kidini isiyoeleweka vizuri. Matokeo ya kazi Yake hayawezi kupatikana kwa mwanadamu ambaye hajakamilishwa na Yeye na yapo nje ya uwezo wa fikira za mwanadamu.

Kazi katika akili ya mwanadamu inafikiwa kwa urahisi sana na mwanadamu. Wachungaji na viongozi katika ulimwengu wa kidini, kwa mfano, wanategemea karama zao na nafasi zao katika kufanya kazi zao. Watu wanaowafuata kwa muda mrefu wataambukizwa na karama zao na kuvutwa na vile walivyo. Wanalenga karama za watu, uwezo na maarifa ya watu, na wanamakinikia mambo ya kimiujiza na mafundisho mengi yasiyokuwa na uhalisi (kimsingi, haya mafundisho ya kina hayawezi kutekelezeka). Hawalengi mabadiliko ya tabia za watu, badala yake wanalenga kuwafundisha watu uwezo wao wa kuhubiri na kufanya kazi, kuboresha

maarifa ya watu na mafundisho yao mengi ya kidini. Hawalengi kuona ni kwa kiasi gani tabia ya watu imebadilika au ni kwa kiasi gani watu wanauelewa ukweli. Wala hawajali kuhusu viini vya watu, wala kujua hali za watu za kawaida na zisizo za kawaida. Hawapingi mitazamo ya watu au kufichua fikira zao, sembuse kuwapogoa watu kwa ajili ya upungufu wao wa dhambi. Wengi wanaowafuata wanahudu kwa vipaji vyao, na yote wanayotoa ni fikira za kidini na nadharia za theolojia, ambazo haziambatani na uhalisi na haziwezi kabisa kuwapa watu uzima. Kwa kweli, kiini cha kazi yao ni kulea talanta, kumlea mtu kuwa mhitimu mwenye talanta aliyemaliza mafunzo ya kidini ambaye baadaye anakwenda kufanya kazi na kuongoza. Kwa miaka elfu sita ya kazi ya Mungu unaweza kupata sheria zozote kuihusu? Kuna kanuni na vizuizi vingi katika kazi ambayo mwanadamu hufanya, na ubongo wa mwanadamu umejazwa na mafundisho mengi ya kidini. Hivyo mwanadamu anachokionyesha ni kiasi cha maarifa na utambuzi ndani ya uzoefu wake wote. Mwanadamu hawezi kuonyesha kitu chochote zaidi ya hiki. Uzoefu au maarifa ya mwanadamu hayaibuki kutoka ndani ya karama zake za ndani au tabia yake; vinaibuka kwa sababu ya uongozi wa Mungu na uchungaji wa moja kwa moja wa Mungu. Mwanadamu ana ogani tu ya kupokea uongozi huu na sio ogani ya kuonyesha moja kwa moja uungu. Mwanadamu hana uwezo wa kuwa chanzo, anaweza kuwa tu chombo ambacho hupokea maji kutoka kwa chanzo; hii ni silika ya mwanadamu, ogani ambayo mtu anapaswa kuwa nayo kama mwanadamu. Ikiwa mtu anapoteza ogani ya kukubali neno la Mungu na kupoteza silika ya kibinadamu, mtu huyo anapoteza pia kile ambacho ni cha thamani sana, na anapoteza wajibu wa mwanadamu aliyeumbwa. Ikiwa mtu hana maarifa au uzoefu wa neno la Mungu au kazi Yake, mtu huyo anapoteza wajibu wake, wajibu anaopaswa kuutimiza kama kiumbe aliyeumbwa, na kupoteza heshima ya kiumbe aliyeumbwa. Ni silika ya Mungu kuonyesha uungu ni nini, kama unaonyeshwa katika mwili au moja kwa moja na Roho Mtakatifu; hii ni huduma ya Mungu. Mwanadamu anaonyesha uzoefu wake mwenyewe au maarifa (yaani, anaonyesha kile alicheo) wakati wa kazi ya Mungu au baada yake; hii ndiyo silika ya mwanadamu na wajibu wa mwanadamu, ndicho kitu ambacho mwanadamu anapaswa kukifikia. Ingawa maonyesho ya mwanadamu ni duni sana kuliko kile ambacho Mungu anaonyesha, na kuna kanuni nyingi katika kile ambacho mwanadamu huonyesha, mwanadamu anapaswa kutimiza wajibu anaopaswa kutimiza na kufanya kile anachopaswa kufanya. Mwanadamu anapaswa kufanya kitu chochote kinachowezekana kwa mwanadamu kufanya ili kutimiza wajibu wake, na hapaswi kuacha kitu hata kidogo.

Baada ya kufanya kazi kwa miaka mingi, mwanadamu atakuwa na uzoefu wa miaka hii yote, vile vile atakuwa na hekima na kanuni alizozipata. Yeye anayefanya kazi kwa muda mrefu anajua jinsi ya kuelewa kusonga kwa Roho Mtakatifu, anajua ni wakati gani Roho Mtakatifu anafanya kazi na wakati gani Hafanyi; anajua jinsi ya kufanya ushirika akiwa amebeba mzigo,

anaitambua hali ya kawaida ya kazi ya Roho Mtakatifu na hali ya kawaida ya ukuaji wa watu katika maisha. Huyu ni mtu ambaye amefanya kazi kwa miaka mingi na anajua kazi ya Roho Mtakatifu. Wale ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu wanazungumza kwa uhakika na bila haraka; hata wakati ambapo hawana kitu cha kusema wanakuwa watulivu. Kwa ndani, wanaweza kuendelea kuomba ili kupata kazi ya Roho Mtakatifu na kupata utiifu wa kweli kwa Mungu; wana uzoefu katika kufanya kazi. Mtu ambaye amefanya kazi kwa muda mrefu na ana masomo na uzoefu mkubwa ana vitu vingi ndani ambavyo vinazuia kazi ya Roho Mtakatifu; hii ni dosari ya kufanya kazi kwa muda mrefu. Mtu ambaye ameanza tu kufanya kazi hajaleta katika kazi masomo au uzoefu wa kibinadamu, hususan kuhusu jinsi ambavyo Roho Mtakatifu anafanya kazi. Hata hivyo, wakati wa kufanya kazi, taratibu anaanza kuelewa jinsi ambavyo Roho Mtakatifu anafanya kazi na anakuwa na utambuzi wa jinsi ya kufanya ili kupata kazi ya Roho Mtakatifu, kile cha kufanya ili kupiga udhaifu wa wengine kabisa, na ufahamu mwingine wa kawaida ambao wale wanaofanya kazi wanapaswa kuwa nao. Kadiri muda unavyokwenda, anapata kujua hekima hiyo na maarifa ya kawaida kuhusu kufanya kazi kwa ufasaha mkubwa sana, na anaonekana kuyatumia kwa urahisi anapofanya kazi. Hata hivyo, Roho Mtakatifu anapobadilisha namna Anavyofanya kazi, bado anakuwa amejikita katika maarifa yake ya zamani ya kufanya kazi na kanuni zake za zamani za kufanya kazi na anajua kidogo sana kuhusu harakati mpya za kufanya kazi. Miaka mingi ya kufanya kazi na kuwa katika uongozi na uwepo kamili wa Roho Mtakatifu kunampa masomo mengi zaidi ya kufanya kazi na uzoefu mwingi. Vitu kama hivyo vinamjaza kujiamini ambako sio kiburi. Kwa maneno mengine, anafurahishwa kabisa na kazi yake mwenyewe na kuridhika sana na maarifa ya kawaida aliyoyapata kuhusu kazi ya Roho Mtakatifu. Hasa, vitu vile ambavyo watu wengine hawakuvipata au kuvitambua vinampatia kujiamini zaidi kwa nafsi yake; inaonesha kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ndani yake haiwezi kuzimwa kamwe, na wengine hawana sifa ya kutendewa hivi. Watu wa aina hii ambao wamefanya kazi kwa miaka mingi na ambao wameitumia thamani ndio wana sifa ya kuifurahia. Vitu hivi vinakuwa ni kikwazo kikubwa katika kukubali kazi mpya ya Roho Mtakatifu. Hata kama anaweza kuikubali kazi mpya, si kitu cha kuibuka mara moja. Kwa uhakika atapitia michakato kadhaa kabla ya kuikubali. Hali hii inaweza kugeuka taratibu baada ya fikira zake za zamani kushughulikiwa na tabia yake ya zamani kuhukumiwa. Bila ya kupitia hatua hizi, habadiliki na kukubali kwa urahisi mafundisho mapya na kazi ambayo haikubaliani na fikira zake za zamani. Hiki ndicho kitu kigumu zaidi kushughulika nacho katika mwanadamu, na sio rahisi kuibadilisha. Ikiwa, kama mtenda kazi, ana uwezo wa kupata na kuelewa kazi ya roho Mtakatifu na kuutambua mchakato wake, vile vile ana uwezo wa kutozuiwa na uwezo wake wa kufanya kazi na kuwa na uwezo wa kuikubali kazi mpya katika mwanga wa kazi ya zamani, ni mtu mwenye hekima na mtenda kazi mwenye sifa. Wanadamu huwa hivi mara nyingi: Wanafanya kazi kwa miaka mingi bila kuweza kufupisha uzoefu wao wa maisha, ama baada ya

kufupisha uzoefu na hekima yao, wanazuiwa kukubali kazi mpya na hawawezi kuelewa kwa usahihi au kuishughulikia kwa usahihi kazi ya zamani na mpya. Wanadamu hakika ni wagumu kuwaongoza! Wengi wenu mko hivi. Wale ambao wamepitia uzoefu wa miaka katika kazi ya Roho Mtakatifu wanaona vigumu kuikubali kazi mpya, mara nyingi wanakuwa wamejazwa mitazamo ambayo wanaona ni vigumu kuiacha, ilhali mtu ambaye ameanza tu kazi anakosa maarifa ya kawaida kuhusu kufanya kazi na hajui hata jinsi ya kushughulikia masuala rahisi kabisa. Nyinyi watu ni wagumu kweli kweli! Wale wenye vyeo fulani nyuma yao wana kiburi na majivuno kweli kiasi kwamba wamesahau kule walikotoka. Siku zote wanawadharau wadogo, ila bado hawawezi kukubali kazi mpya na hawawezi kuachana na fikira walizoikusanya na kuziweka kwa miaka mingi sana. Ingawa hao watu wadogo wasiokuwa na maarifa wanaweza kukubali kiasi kidogo cha kazi ya Roho Mtakatifu na wana shauku kubwa, daima wanachanganyikiwa na hawajui cha kufanya wanapokutana na matatizo. Ingawa wana shauku, wao ni wajinga mno. Wana ufahamu mdogo tu wa kazi ya Roho Mtakatifu na hawawezi kuutumia katika maisha yao; huwa ni mafundisho tu ambayo hayana maana kabisa. Kuna watu wengi kama wewe; ni wangapi wanafaa kwa ajili ya kutumika? Kuna wangapi wanaoweza kutii nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu na waweze kutimiza mapenzi ya Mungu? Inaonekana kwamba wale ambao mmekuwa wafuasi hadi sasa mmekuwa watiifu, lakini kwa kweli, hamjaachana na fikira zenu, bado mnatafuta kwenye Biblia, mkiamini mambo yasiyo dhahiri, au kuzurura katika fikira. Hakuna yeyote ambaye huchunguza kazi halisi ya leo au kuzama ndani yake. Mnaikubali njia ya leo kwa mitazamo yenu ya zamani. Mtafaidika vipi na imani kama hiyo? Inaweza kusemwa kuwa ndani yenu mmefichwa fikira nyingi ambazo zinafichuliwa, na kwamba mnafanya tu jitihada kubwa kuificha na msiweze kuifunua kwa urahisi. Hamkubali kazi mpya kwa uaminifu na hampangi kuachana na fikira zenu za zamani; mna falsafa nyingi sana za kuishi nazo ni kubwa sana. Hamwachi fikira zenu za zamani na kwa shingo upande mnashughulika na kazi mpya. Mioyo yenu ni miovu sana, na hamchukui hatua ya kazi mpya katika moyo. Mtu mzembe kama nyinyi anaweza kufanya kazi ya kueneza injili? Mnaweza kuchukua kazi mpya ya kueneza injili katika ulimwengu mzima? Matendo yenu haya yanawazuia kubadilisha tabia yenu na kumjua Mungu. Mkiendelea hivi, mwisho wake mtaondolewa.

Mnapaswa kujua jinsi ya kutofautisha kazi ya Mungu na kazi ya mwanadamu. Mnaweza kuona nini katika kazi ya mwanadamu? Kuna vitu vingi ambavyo ni uzoefu wa mwanadamu katika kazi ya mwanadamu; kile ambacho mwanadamu anakionyesha kile alichio. Kazi ya Mungu pia inaonyesha kile Alichio, lakini kile Alichio ni tofauti na mwanadamu alivyo. Kile mwanadamu alichio ni kiwakilishi cha uzoefu na maisha ya mwanadamu (kile ambacho mwanadamu anakipitia au kukabiliana nacho katika maisha yake, au falsafa za kuishi alizo

nazo), na watu wanaoishi katika mazingira tofauti huonyesha nafsi tofauti. Kama una uzoefu wa kijamii au la na jinsi ambavyo unaishi na kupitia uzoefu katika familia yako inaweza kuonekana katika kile unachokionyesha, wakati ambapo huwezi kuona kutoka kwa kazi ya Mungu mwenye mwili kama Ana uzoefu wa maisha ya kijamii au Hana. Anatambua vizuri asili ya mwanadamu, Anaweza kufunua aina za matendo yote yanayohusiana na kila aina ya watu. Ni mzuri hata katika kufunua tabia ya dhambi ya mwanadamu na tabia yake ya uasi. Haishi miongoni mwa watu wa kidunia, lakini Anatambua asili ya watu wenye mwili wa kufa na upotovu wote wa watu wa duniani. Hicho ndicho Alichu. Ingawa Hashughuliki na dunia, Anajua kanuni za kushughulika na dunia, kwa sababu Anaielewa vizuri asili ya mwanadamu. Anajua kuhusu kazi ya Roho ambayo jicho la mwanadamu haliwezi kuona na kwamba masikio ya mwanadamu hayawezi kusikia, wanadamu wa leo na wanadamu wa enzi zote. Hii inajumuisha hekima ambayo sio falsafa ya kuishi na makuu ambayo ni ngumu kwa watu kuelewa. Hiki ndicho Alichu, kuwekwa wazi kwa watu na pia kufichika kwa watu. Kile Anachoonyesha sio kile ambacho mwanadamu asiye wa kawaida alichu, bali ni tabia za asili na uungu wa Roho. Hasafiri ulimwenguni mzima lakini anajua kila kitu kuhusu ulimwengu. Anawasiliana na “sokwe” ambao hawana maarifa au akili, lakini Anaonyesha maneno ambayo ni ya kiwango cha juu kuliko maarifa na juu ya watu wakubwa duniani. Anaishi miongoni mwa kundi la wanadamu wapumbavu na wasiojali ambao hawana ubinadamu na ambao hawaelewi mila na desturi za ubinadamu na maisha, lakini Anaweza kumwambia mwanadamu kuishi maisha ya kawaida, na kwa wakati uo huo kufichua ubinadamu duni na wa chini wa binadamu. Haya yote ndiyo kile Alichu, mkuu kuliko vile ambacho mwanadamu yeyote wa damu na nyama alichu. Kwake Yeye, si lazima kupitia maisha ya kijamii magumu na changamani, ili Aweze kufanya kazi Anayotaka kufanya na kwa kina kufichua asili ya mwanadamu aliyepotoka. Maisha duni ya kijamii ambayo hayauadilishi mwili Wake. Kazi Yake na maneno Yake hufichua tu kutotii kwa mwanadamu na hayampi mwanadamu uzoefu na masomo kwa ajili ya kushughulika na ulimwengu. Hahitaji kuipeleleza jamii au familia ya mwanadamu wakati Anapompa mwanadamu uzima. Kumweka wazi na kumhukumu wanadamu sio maonyesho wa uzoefu wa mwili Wake; ni kufichua vile mwanadamu asivyokuwa na haki baada ya kufahamu kutotii kwa mwanadamu na kuchukia upotovu wa mwanadamu. Kazi yote Anayoifanya ni kufichua tabia Yake kwa mwanadamu na kuonyesha asili Yake. Ni Yeye tu ndiye anayeweza kuifanya kazi hii, sio kitu ambacho mtu mwenye mwili na damu anaweza kukipata. Kwa kuangalia kazi Yake, mwanadamu hawezi kuelezea Yeye ni mtu wa aina gani. Mwanadamu hawezi kumwainisha kama mtu aliyeumbwa kwa misingi ya kazi Yake. Kile Alichu pia kinamfanya Asiweze kuainishwa kama mtu aliyeumbwa. Mwanadamu anaweza kumwona tu kama Asiye mwanadamu, lakini hajui amwainishe katika kundi gani, kwa hivyo mwanadamu analazimika kumwainisha katika kundi la Mungu. Si busara kwa mwanadamu kufanya hivi, kwa sababu Amefanya kazi kubwa miongoni

mwa watu, ambayo mwanadamu hawezi kufanya.

Kazi ambayo Mungu anafanya haiwakilishi uzoefu wa mwili Wake; kazi ambayo mwanadamu anafanya inawakalisha uzoefu wa mwanadamu. Kila mtu anazungumza kuhusu uzoefu wake binafsi. Mungu anaweza kuonyesha ukweli moja kwa moja, wakati mwanadamu anaweza tu kuonyesha uzoefu unaolingana na huo baada ya kupata uzoefu wa ukweli. Kazi ya Mungu haina masharti na haifungwi na muda au mipaka ya kijiografia. Anaweza kuonyesha kile Alichokwaki wakati wowote, mahali popote. Anafanya kazi vile Anavyopenda. Kazi ya mwanadamu ina masharti na muktadha; vinginevyo hana uwezo wa kufanya kazi na hawezi kuonyesha ufahamu wake wa Mungu au uzoefu wake wa ukweli. Unatakiwa tu kulinganisha tofauti baina yao ili kuonyesha kama ni kazi ya Mungu mwenyewe au kazi ya mwanadamu. Kama hakuna kazi inayofanywa na Mungu Mwenyewe, na kuna kazi tu ya mwanadamu, utajua tu kwamba mafundisho ya mwanadamu ni makuu, zaidi ya uwezo wa mtu yeyote yule; toni yao ya kuzungumza, kanuni zao katika kushughulikia mambo na uwezo wao katika kufanya kazi ni zaidi ya uwezo wa wengine. Nyinyi nyote mnavutiwa na watu hawa wa ubora mzuri wa tabia na maarifa ya juu, lakini hamwezi kuona kutoka katika kazi na maneno ya Mungu jinsi ubinadamu Wake ulivyo wa juu. Badala yake, Yeye ni wa kawaida, na Anapofanya kazi, Yeye ni wa kawaida na halisi lakini pia hapimiki kwa watu wenye mwili wa kufa, kitu ambacho kinawafanya watu wahisi kumheshimu sana. Pengine uzoefu wa mtu katika kazi yake ni mkubwa sana, au mawazo na fikira zake ni za juu sana, na ubinadamu wake ni mzuri hasa; hivi vinaweza kutamaniwa na watu tu, lakini visiamshe kicho na hofu yao. Watu wote wanawatamani wale ambao wana uwezo wa kufanya kazi na ambao wana uzoefu wa kina na wanaweza kuutenda ukweli, lakini hawawezi kuvuta kicho, bali kutamani na kijicho. Lakini watu ambao wamepitia uzoefu wa kazi ya Mungu hawamtamani Mungu, badala yake wanahisi kwamba kazi Yake haiwezi kufikiwa na mwanadamu na haiwezi kueleweka na mwanadamu, na kwamba ni nzuri na ya kushangaza. Watu wanapopitia uzoefu wa kazi ya Mungu, ufahamu wao wa kwanza kumhusu ni kwamba Yeye ni asiyeleweka, ni mwenye hekima na wa ajabu na wanamcha bila kujua na kuihisi siri ya kazi Anayoifanya, ambayo inapita akili ya mwanadamu. Watu wanataka tu kuwa na uwezo wa kukidhi matakwa Yake, kuridhisha matamano Yake; hawatamani kumpita Yeye, kwa sababu kazi anayoifanya inazidi fikira za mwanadamu na haiwezi kufanywa na mwanadamu kama mbadala. Hata mwanadamu mwenyewe hayajui mapungufu yake, wakati Amefungua njia mpya na kumleta mwanadamu katika dunia mpya zaidi na nzuri zaidi, kwamba mwanadamu amefanya maendeleo mapya na kuwa na mwanzo mpya. Kile ambacho watu wanahisi kumhusu Mungu, sio matamano, au sio matamano tu. Uzoefu wake wa kina ni kicho na upendo, hisia zake ni kwamba Mungu kweli ni wa ajabu sana. Anafanya kazi ambayo mwanadamu hawezi kufanya na kusema mambo ambayo mwanadamu hawezi kusema. Watu ambao wamepitia kazi

ya Mungu daima wana hisia isiyoweza kuelezeka. Watu wenye uzoefu wa kina kutosha wanaweza kuelewa ukweli wa Mungu; wanaweza kuhisi uzuro Wake, kwamba kazi Yake ni ya hekima sana, ya ajabu sana, na hivyo hii inazalisha nguvu isiyokoma ndani yao. Si woga au upendo wa mara moja moja na heshima, bali hisia za ndani za upendo wa Mungu na uvumilivu kwa mwanadamu. Hata hivyo, watu ambao wamepata uzoefu wa kuadibu na hukumu Yake wanamhisi kuwa Yeye mtukufu na asiye kosewa. Hata watu ambao wamepitia uzoefu mkubwa wa kazi Yake pia hawawezi kumwelewa; watu wote wanaomcha wanajua kwamba kazi Yake hailingani na fikira za watu lakini siku zote inakwenda kinyume na fikira zao. Haihitaji watu wamtamani kabisa au kuwa na kuonekana kwa kujikabidhi Kwake, badala yake anataka wawe na uchaji wa kweli na kutii kikamilifu. Katika nyingi ya kazi Yake, mtu yeyote mwenye uzoefu wa kweli anahisi heshima Kwake, ambayo ni ya juu kuliko matamania. Watu wameiona tabia Yake kwa sababu ya kazi Yake ya kuadibu na hukumu, na kwa hiyo wanamcha mioyoni mwao. Mungu anapaswa kuchiwa na kutiwa, kwa sababu uungu Wake na tabia Yake havifanani kama ule wa watu walioumbwa na vikuu juu ya vile vya watu walioumbwa. Mungu hategemei chochote kuwepo na ni wa milele, Yeye siye kiumbe Aliyeumbwa, na ni Mungu tu anayestahili uchaji na utiifu; mwanadamu hana sifa ya kupewa hivi. Hivyo, watu wote waliopitia uzoefu wa kazi Yake na kweli wanamjua wanampatia heshima. Hata hivyo, wale ambao hawaachani fikira zao kumhusu, yaani, wale ambao hawamwoni kuwa Mungu, hawana uchaji wowote Kwake, na hata ingawa wanamfuata hawajashindwa; ni watu wasiotii kwa asili yao. Anafanya kazi hii ili apate matokeo kwamba viumbe vyote vilivyoumbwa vinaweza kumcha Muumbaji, vimwabudu Yeye, na kujikabidhi katika utawala Wake bila masharti. Haya ni matokeo ya mwisho ambayo kazi Yake yote inalenga kuyapata. Ikiwa watu ambao wamepitia kazi hiyo hawamchi Mungu, hata kidogo, kama kutotii kwao kwa zamani hakutabadilika kabisa, basi watu hawa ni hakika wataondolewa. Kama mtazamo wa mwanadamu kwa Mungu ni kumtamani au kuonyesha heshima kwa mbali na sio kumpenda, hata kidogo, hivi ndivyo mtu bila moyo wa kumpenda Mungu anapofikia, na mtu wa aina hiyo anakosa hali za kumwezesha kukamilishwa. Ikiwa kazi nyingi vile haiwezi kupata upendo wa kweli wa mtu, hii ina maana kwamba mtu huyo hajampata Mungu na kwa uhalisi hatafuti kuujua ukweli. Mtu ambaye hampendi Mungu hapendi ukweli na hivyo hawezi kumpata Mungu, sembuse kupata ukubali wa Mungu. Watu kama hao, bila kujali jinsi wanavyopata uzoefu wa Roho Mtakatifu, na bila kujali jinsi gani wanapitia uzoefu wa hukumu, bado hawawezi kumcha Mungu. Hawa ni watu ambao asili yao haiwezi kubadilishwa, ambao wana tabia ya uovu uliokithiri. Wale wote ambao hawamchi Mungu wataondolewa, na kuwa walengwa wa hukumu, na kuadhibiwa kama tu wale ambao wanafanya uovu, watateseka hata zaidi ya wale ambao wamefanya matendo maovu.

Kujua Hatua Tatu za Kazi ya Mungu Ndiyo Njia ya Kumjua

Mungu

Kazi ya kumsimamia mwanadamu imegawanywa katika hatua tatu, na ina maana kuwa kazi ya kumwokoia mwanadamu imegawanywa katika hatua tatu. Hatua hizi tatu hazihusishi kazi ya kuuumba ulimwengu, ila ni hatua tatu za kazi ya Enzi ya Sheria, Enzi ya Neema, na Enzi ya Ufalme. Kazi ya kuiumba dunia ilikuwa kazi ya kusababisha uwepo wa wanadamu wote. Haikuwa kazi ya kumwokoia mwanadamu, na haina uhusiano na kazi ya kumwokoia mwanadamu, kwa kuwa dunia ilipoumbwa mwanadamu hakuwa amepotoshwa na Shetani, na hivyo hakukuwa na haja ya kutekeleza kazi ya kumwokoia mwanadamu. Kazi ya kumwokoia mwanadamu ilianza tu baada ya mwanadamu kupotoshwa na Shetani, na kwa hivyo kazi ya kumsimamia mwanadamu pia ilianza tu punde mwanadamu alipopotoshwa. Kwa maneno mengine, usimamizi wa Mungu wa mwanadamu ulianza kutokana na kazi ya kumwokoia mwanadamu, na wala haukutokana na kazi ya kuiumba dunia. Hakungekuwa na kazi ya kumsimamia mwanadamu pasipo kuwepo na tabia potovu ya mwanadamu, na kwa hivyo kazi ya kumsimamia mwanadamu ina sehemu tatu, badala ya hatua nne, au enzi nne. Hii tu ndio njia sahihi ya kutaja kazi ya Mungu ya usimamizi wa mwanadamu. Enzi ya mwisho itakapofikia kikomo, kazi ya kusimamia mwanadamu itakuwa imekamili. Hitimisho la kazi ya usimamizi lina maana kuwa kazi ya kuwaokoia wanadamu wote imekamili kabisa, na kwamba mwanadamu amefika mwisho wa safari yake. Pasipo kazi ya kuwaokoia wanadamu wote, kazi ya usimamizi wa wanadamu haingekuwapo, wala hakungekuwa na hatua tatu za kazi. Ilikuwa ni hasa kwa ajili ya upotovu wa mwanadamu, na kwa sababu mwanadamu alihitaji wokovu kwa dharura, ndipo Yehova alikamilisha uumbaji wa dunia na kuanza kazi ya Enzi ya Sheria. Hapo tu ndipo kazi ya kumsimamia mwanadamu ilipoanza, kumaanisha kwamba hapo tu ndipo kazi ya kumwokoia mwanadamu ilipoanza. “Kumsimamia mwanadamu” haimaanishi kuongoza maisha ya mwanadamu aliyeumbwa upya duniani (ambapo ni kusema, mwanadamu ambaye bado hakuwa amepotoshwa). Badala yake, ni wokovu wa mwanadamu ambaye amepotoshwa na Shetani, ambapo ni kusema kwamba, ni kubadilishwa kwa mwanadamu aliyepotoshwa. Hii ndiyo maana ya kumsimamia mwanadamu. Kazi ya kumwokoia mwanadamu haihusishi kazi ya kuiumba dunia, na kwa hivyo kazi ya kumsimamia mwanadamu haijumuishi kazi ya kuumba ulimwengu, na inahusisha tu hatua tatu za kazi zilizo tofauti na uumbaji wa ulimwengu. Ili kuelewa kazi ya kumsimamia mwanadamu, ni muhimu kuwa na ufahamu wa historia ya hatua tatu za kazi—hili ndilo kila mtu anapaswa kulifahamu ili kuokolewa. Kama viumbe wa Mungu, mnapaswa kutambua kuwa mwanadamu aliumbwa na Mungu, na kufahamu chanzo cha upotovu wa mwanadamu, na, vilevile, kufahamu mchakato wa wokovu wa mwanadamu. Iwapo mnafahamu tu jinsi ya kutenda kulingana na mafundisho ili kupata neema ya Mungu, lakini hamna fununu jinsi Mungu anavyomwokoia mwanadamu, au ya chanzo cha upotovu wa

mwanadamu, basi hili ndilo mnalokosa kama viumbe wa Mungu. Hupaswi kutoshelezwa tu na kuelewa kwa ukweli unaoweza kuwekwa katika vitendo, huku ukibakia kutojua upeo mpana wa kazi ya usimamizi ya Mungu—kama hivi ndivyo ilivyo, basi wewe ni mwenye kulazimisha kauli sana. Hatua tatu za kazi ya Mungu ndizo hadithi ya ndani ya usimamizi wa Mungu wa mwanadamu, ujio wa injili ya dunia nzima, fumbo kubwa zaidi kati ya wanadamu, na pia ni msingi wa kueneza injili. Ukizingatia tu kuelewa ukweli sahili unaohusiana na maisha yako, na usijue lolote kuhusu hili, maajabu makuu zaidi na maono, basi maisha yako si ni sawa na bidhaa yenye kasoro, yasio na maana isipokuwa kuangaliwa?

Ikiwa mwanadamu huzingatia tu matendo, na kuona kazi ya Mungu na hekima ya mwanadamu kama za upili, basi si ni sawa na kufikira mambo yasiyokuwa muhimu huku ukipuuza mambo yaliyo muhimu zaidi? Lile ambalo sharti ulijue, lazima ulijue, na kile unachostahili kuonyesha kwa vitendo, lazima ukionyeshe kwa vitendo. Ni hapo tu ndipo utakapokuwa mtu anayejua kufuata ukweli. Siku yako ya kueneza injili itakapowadia, ikiwa utaweza kusema tu kuwa Mungu ni Mkuu na Mwenye haki, kuwa ni Mungu Mkuu, Mungu ambaye hapana mwanadamu yeyote mkuu anayeweza kujilinganisha naye, na kuwa hakuna aliye juu zaidi wa kumpiku..., kama waweza tu kusema maneno haya yasiyofaa na ovyo, na kabisa huwezi kunena maneno yenye umuhimu zaidi, na yaliyo na kiini, kama huna lolote la kusema kuhusu kumjua Mungu, ama kazi ya Mungu, na zaidi ya hapo, huwezi kuelezea ukweli, au kutoa kile ambacho kinakosekana kwa mwanadamu, basi mtu kama wewe hana uwezo wa kutekeleza wajibu wake vyema. Kumshuhudia Mungu na kueneza injili ya ufalme si jambo rahisi. Lazima kwanza uwe na ukweli, na maono yatakayoeleweka. Unapokuwa na uwazi wa maono na ukweli wa masuala tofauti ya kazi ya Mungu, moyoni mwako unapata kujua kazi ya Mungu, na bila kujali anayoyafanya Mungu—iwe ni hukumu ya haki ama kusafishwa kwa mwanadamu—unamiliki maono makuu kama msingi wako, na unamiliki ukweli sahihi wa kuonyesha kwa matendo, basi utaweza kumfuata Mungu hadi mwisho. Lazima ujue kuwa bila kujali kazi ambayo Yeye anatenda, lengo la kazi ya Mungu halibadiliki, kiini cha kazi Yake hakibadiliki, na mapenzi Yake kwa mwanadamu hayabadiliki. Bila kujali maneno Yake ni makali namna gani, haijalishi mazingira ni mabaya kiasi gani, kanuni za kazi Yake, na nia Yake ya kumwoko mwanadamu hayatabadilika. Mradi tu si ufunuo wa mwisho wa mwanadamu au hatima ya mwanadamu, na si kazi ya awamu ya mwisho, au kazi ya kutamatisha mpango wote wa usimamizi wa Mungu, na mradi tu ni wakati Anapomfinyanga mwanadamu, basi kiini cha kazi Yake hakitabadilika: Daima kitakuwa wokovu wa mwanadamu. Hili linapaswa kuwa msingi wa imani yenu katika Mungu. Lengo la hatua tatu za kazi ni wokovu wa wanadamu wote—ambayo inamaanisha wokovu kamili wa mwanadamu kutoka kwa miliki ya Shetani. Ingawa kila moja ya hatua ya kazi ina madhumuni na umuhimu, kila moja ni sehemu ya kazi ya kumwoko

mwanadamu, na ni kazi tofauti ya wokovu inayotekelezwa kulingana na matakwa ya mwanadamu. Punde unapofahamu lengo la hatua hizi tatu za kazi, basi utafahamu jinsi ya kuthamini umuhimu wa kila hatua ya kazi, na utatambua jinsi ya kutenda ili kutosheleza shauku ya Mungu. Iwapo utaweza kufikia hatua hii, basi hili, ono kubwa kuliko yote, litakuwa msingi wa imani yako katika Mungu. Unapaswa kufuata sio tu njia rahisi za matendo, ama ukweli wenye undani, lakini unapaswa kuunganisha maono na matendo, ili kwamba kuwe na ukweli unaoweza kuwekwa kwenye vitendo, na maarifa yaliyo na msingi wa maono. Ni hapo tu ndipo utakapokuwa mtu anayefuatilia ukweli.

Hatua tatu za kazi ndizo kiini cha usimamizi mzima wa Mungu, na ndani yazo zimeelezwa tabia ya Mungu na kile Alichu. Wale wasiojua kuhusu hatua tatu za kazi ya Mungu hawana uwezo wa kutambua jinsi Mungu anavyoonyesha tabia Yake, wala hawajui hekima ya kazi ya Mungu, na wanasalia kutojua njia nyingi Anazomwokoa mwanadamu, na mapenzi Yake kwa wanadamu wote. Hatua tatu za kazi ndizo maonyesho kamili ya kazi ya kumwokoa mwanadamu. Wale wasiofahamu hatua tatu za kazi watakosa kuelewa njia mbalimbali na kanuni za kazi ya Roho Mtakatifu; wale wanaoshikilia tu imara mafundisho ya dini yanayosalia kutoka katika hatua moja ya kazi ni watu wanaomwekea Mungu mipaka kwa mafundisho ya dini, na wale ambao imani yao kwa Mungu haina udhahiri na uhakika. Watu kama hao kamwe hawawezi kupokea wokovu wa Mungu. Ni hatua tatu tu za Mungu zinazoweza kuonyesha kabisa ukamilifu wa tabia ya Mungu, na kuonyesha kabisa nia ya Mungu ya kuwaokoa wanadamu wote, na mchakato mzima wa wokovu wa mwanadamu. Hili ni dhibitisho kuwa Yeye amemshinda Shetani na kumpata mwanadamu, ni dhibitisho la ushindi wa Mungu, na ni maonyesho ya tabia kamili ya Mungu. Wale wanaoelewa hatua moja tu kati ya hatua tatu za kazi ya Mungu wanajua tu sehemu ya tabia ya Mungu. Katika dhana ya mwanadamu, ni rahisi kwa hatua hii moja kuwa mafundisho ya kidini, panakuwa na uwezekano zaidi wa mwanadamu kuweka amri kumhusu Mungu, na mwanadamu anatumia hii sehemu moja ya tabia ya Mungu kama dhihirisho la tabia nzima ya Mungu. Zaidi ya hayo, mawazo mengi ya mwanadamu yanachanganywa ndani yake, hivi kwamba anaweza vikwazo imara kwa tabia, nafsi, na hekima ya Mungu, na pia kanuni za kazi ya Mungu ndani ya vigezo vyenye mipaka, akiamini kwamba ikiwa Mungu alikuwa hivi wakati mmoja, basi Yeye atasalia kuwa vile daima, na kamwe hatabadilika. Ni wale tu wanaojua na kuthamini hatua tatu za kazi ndio wanaoweza kumjua Mungu kabisa na kwa usahihi. Angalau, hawatamfafanua Mungu kama Mungu wa Waisraeli, ama Wayahudi, na hawatamwona kama Mungu atakayesulubiwa msalabani milele kwa ajili ya mwanadamu. Kama unapata kumjua Mungu kutokana na hatua moja ya kazi Yake tu, basi maarifa yako ni kidogo, kidogo sana. Maarifa yako ni sawa na tone moja katika bahari. Kama si hivyo, kwa nini wengi wa walinzi wa kidini wa kale walimtundika Mungu msalabani akiwa hai? Je, si kwa ajili mwanadamu

humwekea Mungu mipaka kwenye vigezo fulani? Je, si watu wengi humpinga Mungu na kuzuia kazi ya Roho Mtakatifu kwa sababu hawajui kazi mbalimbali na tofautitofauti ya Mungu, na, zaidi ya hayo, kwa sababu wanamiliki maarifa na mafundisho duni ya kupima kazi ya Roho Mtakatifu? Ingawa uzoefu wa watu kama hawa ni wa juujuu tu, ni wenye majivuno na wadekezi katika asili yao, na wanatazama kazi ya Roho Mtakatifu kwa dharau, wanapuuza masomo ya Roho Mtakatifu na, hata zaidi, wanatumia hoja zao ndogo ndogo zee kudhibitisha kazi ya Roho Mtakatifu. Pia wanajifanya, na wanashawishika kabisa na elimu yao na maarifa yao, na kuwa wanaweza kusafiri duniani kote. Je, watu hawa si ni wale wanaochukiwa na kukataliwa na Roho Mtakatifu na je, si wataondolewa na enzi mpya? Je, si wale wanaokuja mbele ya Mungu na kumpinga waziwazi ni watu wadogo wasiojua na wasio na habari ya kutosha jinsi na wanajaribu kuonyesha walivyo werevu? Kwa maarifa haba ya Biblia, wanajaribu kupotosha “wasomi”; wa dunia, kwa mafundisho duni ya dini ili kuwafunza watu, wanajaribu kurudisha nyuma kazi ya Roho Mtakatifu, na kujaribu kuifanya ihusu mchakato wao wanavyofikiria, na kwa kuwa hawaoni mbali, wanajaribu kuona kwa mtazamo mmoja miaka 6,000 ya kazi ya Mungu. Watu hawa hawana mantiki yoyote hata kidogo! Kwa kweli, maarifa ya watu kumhusu Mungu yanavyozidi kuwa mengi, ndivyo wanavyokuwa wagumu wa kuhukumu kazi Yake. Zaidi ya hayo, wanazungumzia tu machache kuhusu maarifa yao ya kazi ya Mungu leo, lakini si wepesi wa kuhukumu. Kadri watu wanavyojua machache kumhusu Mungu, ndivyo wanavyozidi kuwa wenye majivuno na wenye kujiamini sana, na ndivyo wanavyozidi kutangaza nafsi ya Mungu kwa utundu—ilhali wanazungumzia tu nadharia, na wala hawapeani ushahidi wowote halisi. Watu kama hawa hawana thamani yoyote kabisa. Wale wanaoona kazi ya Roho Mtakatifu kama mchezo ni wenye upuzi! Wale wasio waangalifu wanapokumbana na kazi mpya ya Roho Mtakatifu, wanaopayuka, ni wepesi wa kuhukumu wanaoruhusu silika yao ya kiasili kukana haki ya kazi ya Roho Mtakatifu, na pia kuitusi na kuikufuru—je, watu hawa wasio na heshima si ni wale wasiojua kazi ya Roho Mtakatifu? Je, si wao ndio, zaidi ya hayo, wale wasiojua, wenye majivuno ya asili na wasioweza kutawalwa? Hata ikiwa siku itakuja ambapo watu hawa watakubali kazi mpya ya Roho Mtakatifu, bado Mungu hatawavumilia. Hawadharau tu wale wanaofanya kazi ya Mungu, bali pia wanamkufuru Mungu Mwenyewe. Watu kama hawa jasiri pasi na hadhari hawatasamehewa, katika enzi hii ama enzi itakayokuja na wataangamia kuzimuni milele! Watu kama hawa wasio na heshima, wenye kujifurahisha, wanajifanya kuwa wanamwamini Mungu, na kadiri wanavyozidi kufanya vile, ndivyo wanavyozidi kukosea amri za utawala wa Mungu. Je, si hao mafidhuli ambao kiasili hawazuiliki, na hawajawahi kumtii yeyote, wote hupitia njia hii? Je, si wao humpinga Mungu siku baada ya siku, Yeye ambaye daima huwa mpya na wala hazeeki? Leo, mnapaswa kuelewa mbona lazima mjue umuhimu wa hatua tatu za kazi ya Mungu. Maneno Ninayosema yana manufaa kwenu, wala si mazungumzo ya bure. Ukiyasoma tu kama mtu anayetazama na kupendezwa na maua anapoendesha farasi

shoti, si bidii Yangu yote itakuwa kazi bure? Kila mmoja wenu anapaswa kujua asili yake. Wengi wenu wamebobeza katika mabishano, majibu ya maswali ya nadharia yanatoka kinywani mwenu, lakini hamna la kusema kwa maswali kuhusu dutu. Hadi leo, bado mnashiriki mazungumzo duni, na hamuwezi kubadilisha asili yenu ya zamani, na wengi wenu hawana nia ya kubadilisha jinsi mnavyofuatilia ili kupata ukweli wa juu, mnaishi tu maisha yenu shingo upande. Je, watu kama hawa wataweza kumfuata Mungu hadi tamati vipi? Hata ikiwa mtafika mwishoni mwa safari, itakuwa na faida gani kwenu? Ni bora mbadili mawazo yenu kabla hamjachelewa, kufuatilia kwa kweli, au kujitoa mapema. Muda unapokatika utakuwa kimelea doezi—je, mko radhi kutekeleza jukumu kama hili la hali ya chini na lenye aibu?

Hatua tatu za kazi ni rekodi ya kazi nzima ya Mungu, ni rekodi ya wokovu wa Mungu wa mwanadamu, na si porojo tu. Kama kweli mnataka kutafuta kujua tabia nzima ya Mungu, basi sharti mfahamu hatua tatu za kazi inayofanywa na Mungu, na, zaidi, sharti msiache hatua yoyote. Hiki ndicho kiwango cha chini kinachopaswa kufikiwa na wale wanaotafuta kumjua Mungu. Mwanadamu mwenyewe hawezi kuvumbua maarifa ya Mungu. Si kitu ambacho mwanadamu mwenyewe anaweza kufikiria, wala si matokeo ya fadhila za Roho Mtakatifu kwa mtu mmoja. Badala yake, ni maarifa yanayotokea mwanadamu anapopitia kazi ya Mungu, na ni maarifa ya Mungu yanayotokana tu na mwanadamu kupitia ukweli wa kazi ya Mungu. Maarifa kama haya hayawezi kutimizwa kwa ghafla, wala si jambo linaloweza kufundishwa. Inahusiana kabisa na uzoefu wa kibinafsi. Wokovu wa Mungu wa mwanadamu ndiyo kiini cha hatua hizi tatu za kazi, ilhali katika kazi ya wokovu kumejumuishwa mbinu kadhaa za kufanya kazi na namna ambazo tabia ya Mungu imeonyeshwa. Hili ndilo jambo gumu sana kwa mwanadamu kutambua na kwa mwanadamu kuelewa. Mgawanyiko wa enzi, mabadiliko ya kazi ya Mungu, mabadiliko katika eneo la kazi, mabadiliko ya wanaopokea kazi na kadhalika—haya yote yamejumuishwa katika hatua tatu za kazi. Hhususan, tofauti katika njia ya utendakazi wa Roho Mtakatifu, na vilevile mabadiliko katika tabia ya Mungu, picha, jina, utambulisho, au mabadiliko mengine, yote ni sehemu ya hatua tatu za kazi. Sehemu moja ya kazi inaweza tu kuwakilisha sehemu moja, na imewekewa mipaka ndani ya wigo fulani. Haihusiani na mgawanyiko wa enzi, ama mabadiliko ya kazi ya Mungu, wala masuala mengine. Huu ni ukweli ulio waziwazi. Hatua tatu za kazi ya Mungu ndizo ukamilifu wa kazi ya Mungu ya kumwokoza mwanadamu. Mwanadamu lazima ajue kazi ya Mungu, tabia ya Mungu katika kazi ya wokovu, na bila ukweli huu, maarifa yako kumhusu Mungu yatakuwa tu maneno matupu, ni mahubiri ya starehe tu. Maarifa kama haya hayawezi kumshawishi au kumshinda mtu, maarifa kama haya yako nje ya uhalisi, na si ukweli. Yanaweza kuwa mengi, na mazuri kwa masikio, lakini kama hayaambatani na tabia ya asili ya Mungu, basi Mungu hatakusamehe. Hatakosha kuyasifu maarifa yako tu, bali pia atakuadhibu kwa kuwa mwenye dhambi aliyemkufuru. Maneno ya kumjua Mungu hayazungumzwi kwa

mzaha. Ingawa unaweza kuwa na ulimi laini wenye maneno matamu, na ingawa maneno yako ni ya werevu kiasi kwamba unaweza kubishana kitu kisichowezezana, bado huna elimu ya kuzungumza kuhusu maarifa ya Mungu. Mungu si mtu ambaye unaweza kuhukumu kwa urahisi, ama kusifu bila mpango, ama kupaka tope bila kujali. Unamsifu mtu yeyote na watu wowote, ilhali unajitahidi kupata maneno sahihi ya kuelezea ukuu wa wema na neema za Mungu—hili ndilo mshindwa yeyote hujifunza. Ingawa kuna wataalam wengi wa lugha wanaoweza kumwelezea Mungu, usahihi wa kile wanachoelezea ni asilimia moja ya ukweli unaozungumzwa na watu wa Mungu na wana misamiati michache tu, ilhali wanamiliki tajriba yenye uzito. Basi inaweza kuonekana kuwa maarifa ya Mungu yapo katika usahihi na uhalisi, na wala si utumiaji mzuri wa maneno au misamiati mingine, na kwamba maarifa ya mwanadamu na maarifa ya Mungu kabisa hayahusiani. Somo la kumjua Mungu liko juu zaidi kuliko sayansi za asili za mwanadamu. Ni somo linaloweza kutimizwa tu na idadi ndogo sana ya watu wanaotafuta kumjua Mungu, na haliwezi kutimizwa na mtu yeyote tu mwenye kipaji. Na kwa hivyo lazima msione kumjua Mungu na kufuatilia ukweli kama kwamba kunaweza kupatikana na mtoto mdogo tu. Pengine umekuwa na mafanikio makuu katika maisha yako ya kifamilia, ama kazi yako, ama katika ndoa yako, lakini inapofika kwenye ukweli, na somo la kumjua Mungu, huna lolote la kujivunia, hujatimiza malengo yoyote. Kutia ukweli kwenye vitendo, inaweza kusemwa, ni jambo gumu kwenu, na kumjua Mungu ni tatizo kuu hata zaidi. Hili ni tatizo lenu, na pia ni tatizo linalokabiliwa na wanadamu wote. Kati ya wale wenye mafanikio katika kumjua Mungu, karibu wote hawajafikia kiwango. Mwanadamu hajui maana ya kumjua Mungu, ama kwa nini ni muhimu kumjua Mungu, ama kiasi kipi kinahesabiwa kama kumjua Mungu. Hili ndilo linalomshangaza mwanadamu, na ni kitendawili kikubwa zaidi kinachokabiliwa na mwanadamu—na hakuna awezaye kujibu swali hili, ama aliye na hiari kujibu hili swali, kwa sababu, hadi leo, hamna katika wanadamu aliyefanikiwa katika kusomea kazi hii. Pengine, kitendawili cha hatua tatu za kazi kitakapotambulishwa kwa mwanadamu, kutakuwepo katika mfululizo kundi la watu wenye vipaji wanaomjua Mungu. Bila shaka, Natumaini kuwa hivyo ndivyo ilivyo, na, hata zaidi, Niko katika harakati ya kutekeleza kazi hii, na Ninatumaini kuona kujitokeza kwa vipaji zaidi kama hivi katika siku za hivi karibuni. Watakuwa wale wanaoshuhudia ukweli wa hatua hizi tatu za kazi, na, bila shaka, watakuwa pia wa kwanza kushuhudia hizi hatua tatu za kazi. Kama kutakuwa na aliye na vipaji hivi, siku ambayo kazi ya Mungu itafikia kikomo, ama kuwe na wawili ama watatu, na kibinafsi wamekubali kufanywa wakamilifu na Mungu mwenye mwili, basi hakuna jambo la kuhuzunisha na kujutia kama hili—ingawa ni katika hali mbaya zaidi tu. Kwa vyovyote vile, Ninatumai kuwa wale wote wanaotafuta kwa kweli wanaweza kupata baraka hii. Tangu mwanzo wa wakati, hakujawahi kuwa na kazi kama hii, hapo awali hakujawahi kuwa na kazi kama hii katika historia ya ukuaji wa mwanadamu. Kama kweli unaweza kuwa mmoja wa wale wa kwanza wanaomjua Mungu, je,

si hii itakuwa heshima ya juu kuliko viumbe wote? Je, kuna kiumbe mwingine kati ya wanadamu anayeweza kusifiwa na Mungu zaidi? Kazi kama hii ni ngumu kutekeleza, lakini mwishowe bado itapokea malipo. Bila kujali jinsia yao ama uraia wao, wale wote wenye uwezo wa kufikia maarifa ya Mungu, mwishowe, watapokea heshima kuu ya Mungu, na watakuwa tu wenye kumiliki mamlaka ya Mungu. Hii ndiyo kazi ya leo, na pia ndiyo kazi ya siku za usoni; ni ya mwisho na ya juu zaidi kuwahi kutekelezwa katika miaka 6000 ya kazi, na ni njia ya kufanya kazi inayodhihirisha kila kundi la mwanadamu. Kupitia kazi ya kumfanya wanadamu kumjua Mungu, daraja tofauti za mwanadamu zinadhihirishwa: Wale wanaomjua Mungu wamehitimu kupokea baraka za Mungu na kukubali ahadi zake, wakati wale wasiomjua Mungu hawajahitimu kupokea baraka za Mungu wala kupokea ahadi zake. Wale wanaomjua Mungu ni wandani wa Mungu, na wale wasiomjua Mungu hawawezi kuitwa wandani wa Mungu; wandani wa Mungu wanaweza kupokea baraka zozote za Mungu, lakini wale wasio wandani wa Mungu hawastahili kazi yoyote Yake. Iwe ni dhiki, usafishaji, ama hukumu, yote ni kwa ajili ya kumfanya mwanadamu hatimaye kufikia maarifa ya Mungu na ili kwamba mwanadamu amtii Mungu. Hii ndiyo athari pekee itakayofikiwa hatimaye. Hakuna lolote katika hatua tatu za kazi lililofichwa, na hii ni faida kwa maarifa ya mwanadamu kuhusu Mungu, na humsaidia mwanadamu kupata maarifa kamili na mengi ya Mungu. Kazi hii yote ni ya kumfaidi mwanadamu.

Kazi ya Mungu Mwenyewe ni maono ambayo mwanadamu lazima afahamu, kwa kuwa kazi ya Mungu haiwezi kutekelezwa na mwanadamu, wala haimilikiwi na mwanadamu. Hatua tatu za kazi ndizo ukamilifu wa usimamizi wa Mungu, na hakuna ono kuu kuliko hili linalopaswa kufahamika kwa mwanadamu. Kama mwanadamu hafahamu maono haya makuu, basi si rahisi kumjua Mungu, na si rahisi kujua mapenzi ya Mungu, na, zaidi ya hayo, njia ambayo mwanadamu anapitia inazidi kuwa ngumu. Bila maono, mwanadamu hangeweza kufika umbali huu. Ni maono ambayo yamemlinda mwanadamu hadi leo, na ambayo yamempa mwanadamu ulinzi mkuu. Katika siku za usoni, maarifa yenu lazima yawe ya kina, na sharti mfahamu mapenzi Yake yote na umuhimu wa kazi Yake yenye busara katika hatua tatu za kazi. Hiki tu ndicho kimo chenu cha kweli. Hatua ya kazi ya mwisho haisimami peke yake, ila ni sehemu ya yote iliyounganishwa pamoja na hatua mbili za awali, ambayo ni kusema kwamba haiwezekani kukamilisha kazi nzima ya wokovu kwa kufanya kazi ya hatua moja pekee. Ingawa hatua ya mwisho ya kazi inaweza kumwokoia mwanadamu kabisa, hii haimaanishi kwamba ni muhimu tu kutekeleza hatua hii pekee, na kwamba hatua mbili za hapo awali hazihitajiki kumwokoia mwanadamu kutokana na ushawishi wa Shetani. Hakuna hatua moja kati ya zote tatu inayoweza kuwekwa kama maono ya kipekee ambayo lazima yajulishwe mwanadamu, kwa kuwa ukamilifu wa kazi ya wokovu ni hatua tatu za kazi, wala si hatua moja kati ya tatu. Ilimradi kazi ya wokovu bado haijakamilishwa, usimamizi wa Mungu utashindwa kufikia kikomo. Nafsi

ya Mungu, tabia, na hekima zimeonyeshwa katika ukamilifu wa kazi ya wokovu, wala hazikufichuliwa kwa mwanadamu hapo mwanzo, lakini zimeonyeshwa hatua kwa hatua katika kazi ya wokovu. Kila hatua ya kazi ya wokovu huonyesha sehemu ya tabia ya Mungu, na sehemu ya nafsi Yake: si kila hatua ya kazi inayoweza moja kwa moja kuonyesha kabisa na kwa ukamilifu nafsi ya Mungu. Kwa hivyo, kazi ya wokovu inaweza tu kuhitimishwa hatua tatu za kazi zitakapokamilika, na kwa hivyo, maarifa ya mwanadamu ya ukamilifu wa Mungu hayawezi kutenganishwa na hatua tatu za kazi ya Mungu. Kile ambacho mwanadamu hupokea kutoka kwa hatua moja ya kazi ni tabia ya Mungu inayoonyeshwa katika sehemu moja ya kazi yake tu. Haiwezi kuwakilisha tabia na nafsi inayoonyeshwa katika hatua ya awali na ijayo. Hii ni kwa sababu kazi ya kumwokoza mwanadamu haiwezi kumalizika mara moja katika kipindi kimoja, ama katika eneo moja, lakini hukuwa kwa kina hatua kwa hatua kulingana na kiwango cha kukua kwa mwanadamu katika wakati na maeneo tofauti. Ni kazi inayofanywa hatua kwa hatua, na haikamilishwi katika hatua moja. Na kwa hiyo, hekima yote ya Mungu imejumuishwa katika hatua tatu, badala ya hatua moja. Nafsi yake yote na hekima yake yote zimewekwa wazi katika hatua hizi tatu, na kila hatua ina nafsi Yake, na ni rekodi ya hekima ya kazi Yake. Mwanadamu anapaswa kujua tabia yote ya Mungu iliyoonyeshwa katika hatua hizi tatu. Nafsi hii ya Mungu ndiyo ina maana zaidi kwa wanadamu wote, na ikiwa watu hawana maarifa haya wanapomwabudu Mungu, basi hawana tofauti na wale wanaoabudu Budha. Kazi ya Mungu kati ya wanadamu haijafichiwa mwanadamu, na inapaswa kujulikana na wale wote wanaomwabudu Mungu. Kwa sababu Mungu ametekeleza hatua tatu za kazi ya wokovu kati ya wanadamu, mwanadamu anapaswa kujua maonyesho ya kile Anacho na alichwa wakati wa hatua hizi tatu za kazi. Hili ndilo ambalo ni lazima lifanywe na mwanadamu. Kile ambacho Mungu anamfichia mwanadamu ni kile ambacho mwanadamu hawezi kutimiza, na kile ambacho mwanadamu hapaswi kujua, ilhali yale Mungu anayomfunulia mwanadamu ni yale ambayo mwanadamu anapaswa kujua na yale ambayo mwanadamu anapaswa kumiliki. Kila moja ya hatua tatu za kazi huendelea juu ya msingi wa hatua iliyopita; haitekelezwi peke yake, tofauti na kazi ya wokovu. Ingawa kuna tofauti kubwa katika enzi na aina ya kazi ambayo inafanywa, katika kiini chake bado ni wokovu wa mwanadamu, na kila hatua ya kazi ya wokovu ina kina kuliko iliyopita. Kila hatua inaendelea kutoka kwa msingi wa hatua ya mwisho ambayo haiondolewi. Kwa njia hii, katika kazi Yake ambayo daima huwa mpya na kamwe si kuukuu, Mungu mara kwa mara anaonyesha vipengele vya tabia Yake ambavyo havijawahi kuonyeshwa kwa mwanadamu hapo awali, na daima anamfichulia mwanadamu kazi Yake mpya, na nafsi Yake mpya, na hata ikiwa wazoefu wakongwe wa kidini hufanya juu chini kukinzana na hili, na kulipinga waziwazi, Mungu daima hufanya kazi mpya ambayo anakusudia kufanya. Kazi Yake daima hubadilika, na kwa sababu hii, daima inakabiliwa na upinzani wa mwanadamu. Na hivyo, pia, tabia Yake inabadilika daima, na vilevile enzi na wanaopokea kazi Yake. Zaidi ya hayo, kila mara Yeye

hufanya kazi ambayo haijawahi kufanywa tena, hata kufanya kazi ambayo huonekana kwa mwanadamu kuhitilafiana na kazi iliyofanywa awali, kuwa kinyume nayo. Mwanadamu anaweza kukubali tu aina moja ya kazi, ama njia moja ya matendo. Ni vigumu kwa wanadamu kukubali kazi ama njia za matendo, ambayo yanakinzana nao, ama yaliyo juu kuwaliko—lakini Roho Mtakatifu daima anafanya kazi mpya, na kwa hivyo kunakuwepo kikundi baada ya kikundi cha wataalamu wa kidini wanaoipinga kazi mpya ya Mungu. Watu hawa wamekuwa wataalamu hasa kwa sababu mwanadamu hana maarifa ya jinsi Mungu huwa mpya wala hazeeki, na zaidi ya hayo, hana maarifa ya kanuni za kazi ya Mungu, na hata zaidi hawana maarifa ya njia nyingi ambazo Mungu humwokoza mwanadamu. Kwa hivyo, mwanadamu kabisa anashindwa kueleza kama ni kazi inayotoka kwa Roho Mtakatifu, au ni kazi ya Mungu Mwenyewe. Watu wengi hushikilia mtazamo ambao, kama inalingana na maneno yanayokuja kabla, basi wanaweza kuikubali, na kama kuna tofauti na kazi ya awali, basi wanaipinga na kuikataa. Leo, je, nyote hamjafuata katika kanuni hizi? Hatua tatu za kazi ya wokovu hazijakuwa na athari kubwa kwenu, na kuna wale wanaoamini kuwa hatua mbili zilizopita za kazi ni mzigo usiohitaji kufahamika. Wanafikiria kuwa hatua hizi hazifai kutangazwa kwa umati na zinafaa kufutwa haraka iwezekanavyo, ili watu wasihisi kwamba wamezidiwa na hatua mbili za awali za zile hatua tatu za kazi. Wengi wanaamini kuwa kupeana ufahamu kuhusu hatua mbili zilizopita ni hatua ya mbali sana, wala haina faida katika kumjua Mungu—hivyo ndivyo mnayofikiria. Leo, nyote mnaamini kuwa ni haki kutenda vile, lakini siku itawadia ambapo mtagundua umuhimu wa kazi Yangu: Mjue kuwa Sifanyi kazi yoyote ambayo haina umuhimu. Kwa sababu Ninawatangazia hatua tatu za kazi, kwa hivyo lazima ziwe na faida kwenu; kwa sababu hatua hizi tatu za kazi ndizo kiini cha usimamizi mzima wa Mungu, kwa hivyo lazima ziwe lengo la kila mmoja duniani. Siku moja, nyote mtagundua umuhimu wa kazi hii. Fahamuni kuwa mnapinga kazi ya Mungu, ama mnatumia dhana zenu kupima kazi ya leo, kwa sababu hamjui kanuni za kazi ya Mungu, na kwa sababu hamchukulii kazi ya Roho Mtakatifu kwa makini kutosha. Upinzani wenu kwa Mungu na kuzuia kazi ya Roho Mtakatifu kumetokana na dhana zenu na upumbavu wenu wa kiasili. Si kwa sababu kazi ya Mungu si sawa, lakini ni kwa sababu mna tabia ya kiasili ya kutotii. Baada ya kupata imani yao katika Mungu, watu wengine hawawezi hata kusema kwa uhakika mwanadamu alikotoka, ilhali wanathubutu kuzungumza hadharani wakitathmini haki na makosa ya kazi ya Roho Mtakatifu. Na pia wanawakemea mitume ambao wana kazi mpya ya Roho Mtakatifu, wakitoa maoni huku wakizungumza kwa zamu; ubinadamu wao uko chini sana, na hawana hisia zozote. Je, si siku itawadia ambapo watu kama hawa watakataliwa na kazi ya Roho Mtakatifu, na kuchomwa katika moto wa kuzimu? Hawafahamu kazi ya Mungu, lakini badala yake wanakosoa kazi Yake, na pia wanajaribu kumwagiza Mungu jinsi atakavyofanya kazi. Je, ni kwa namna gani watu hawa wasio na busara watamjua Mungu? Mwanadamu huja kumjua Mungu wakati anapomtafuta na anapokuwa na

uzoefu naye; si katika kumkosoa kwa ghafla ndipo anapokuja kumjua Mungu kwa kupitia kutiwa nuru na Roho Mtakatifu. Kadiri maarifa ya watu kuhusu Mungu yanavyozidi kuwa sahihi, ndivyo upinzani wao Kwake unavyopungua. Kinyume na hayo, kadri watu wanavyomjua Mungu kwa kiasi kidogo, ndivyo wanavyokuwa na uwezekano wa kumpinga. Dhana zako, ubinadamu wako wa zamani, na utu wako, tabia na maadili ndiyo “mtaji” ambao unampingia Mungu, na kadri unavyokuwa mpotovu, ama ulivyoshushwa heshima na ulivyo duni, ndivyo unavyozidi kuwa adui wa Mungu. Wale waliomilikiwa na dhana kali na wenye tabia ya unafiki wamo hata zaidi katika uadui wa Mungu mwenye mwili, na watu kama hawa ni wapinga Kristo. Ikiwa dhana zako hazitarekebisha, basi daima zitakuwa kinyume na Mungu; daima hutalingana na Mungu, na daima utakuwa mbali na Yeye.

Ni katika kuweka dhana zako za kale kando tu ndipo utakapoweza kupata maarifa mapya, ilhali maarifa ya zamani si lazima yawe dhana za zamani. “Dhana” inamaanisha vitu vinavyodhaniwa na mwanadamu ambavyo viko mbali na uhalisi. Kama maarifa ya zamani yalikuwa yamepitwa na wakati katika enzi ya kale, na yalimzuia mwanadamu kuingia katika kazi mpya, basi maarifa kama yale pia ni dhana. Ikiwa mwanadamu ataweza kuchukua mwelekeo mzuri kwa maarifa kama yale, na anaweza pata kumjua Mungu kutoka kwa vipengele tofauti, kuunganisha ya zamani na mapya, basi maarifa ya kale yatamsaidia mwanadamu, na yatakuwa msingi wa mwanadamu kuingia katika enzi mpya. Funzo la kumjua Mungu linahitaji kwamba uwe stadi wa kanuni nyingi: jinsi ya kuingia kwenye njia ya kumjua Mungu, ukweli gani unapaswa kuelewa ili kumjua Mungu, na jinsi ya kuondoa dhana zako na asili yako ya kale ili kwamba uweze kutii mipango yote ya kazi mpya ya Mungu. Ukitumia kanuni hizi kama msingi wa kuingia kwenye somo la kumjua Mungu, basi maarifa yako yatakuwa na kina zaidi na zaidi. Kama una maarifa wazi ya hatua tatu za kazi—ambayo ni kusema kwamba, ya mpango mzima wa usimamizi wa Mungu—na ikiwa utaweza kupatanisha hatua mbili za awali na hatua ya sasa, na unaweza kuona kwamba ni kazi iliyofanywa na Mungu mmoja, basi utakuwa na msingi imara zaidi. Hatua tatu za kazi zilifanywa na Mungu mmoja; haya ndiyo maono makubwa zaidi, na ndiyo njia ya pekee ya kumjua Mungu. Hatua tatu za kazi zingefanywa tu na Mungu Mwenyewe, na hapana mwanadamu yeyote ambaye angeweza kufanya kazi kama hii kwa niaba Yake—ambayo ni kusema kuwa ni Mungu Mwenyewe pekee ambaye angeifanya kazi Yake toka mwanzo hadi leo. Ingawa hatua tatu za kazi ya Mungu zimefanywa katika enzi tofauti na maeneo tofauti, na ingawa kazi ya kila moja ni tofauti, yote ni kazi iliyofanywa na Mungu mmoja. Kati ya maono yote, hili ndilo kuu zaidi ambalo mwanadamu anapaswa kulijua, na ikiwa litaeleweka kabisa na mwanadamu, basi ataweza kusimama imara. Leo, tatizo kuu linalokumba dini na madhehebu kadhaa ni kwamba hazijui kazi ya Roho Mtakatifu, na hazina uwezo wa kutofautisha kati ya kazi ya Roho Mtakatifu na kazi isiyo ya Roho Mtakatifu—na kwa hivyo hawawezi

kueleza kama hatua hii ya kazi, kama hatua mbili za awali, pia zimefanywa na Yehova Mungu. Ingawa watu wanamfuata Mungu, wengi hawawezi kueleza kama ni njia sahihi. Mwanadamu anahofia ikiwa hii ndiyo njia inayoongozwa na Mungu Mwenyewe, na kama Mungu kupata mwili ni jambo la hakika, na watu wengi bado hawana dokezo jinsi ya kupambanua ikifikia maneno kama haya. Wale wanaomfuata Mungu hawawezi kujua njia, na kwa hivyo habari zinazozungumzwa zinaathiri sehemu ndogo tu kati ya watu hawa na hayana uwezo wa kufaa kikamilifu, na kwa hivyo, hili basi linaathiri kuingia kwa maisha kwa watu kama hawa. Ikiwa mwanadamu anaweza kuona katika hatua tatu za kazi kuwa zilitekelezwa na Mungu Mwenyewe wakati tofauti, katika maeneo tofauti, na kwa watu tofauti; ikiwa mwanadamu anaweza kuona kuwa ingawa kazi ni tofauti, yote imefanywa na Mungu mmoja, na kwa kuwa ni kazi ambayo imefanywa na Mungu mmoja, basi lazima iwe sawa, na bila dosari, na kwamba ingawa hailingani na dhana za mwanadamu, hakuna kupinga kuwa ni kazi iliyofanywa na Mungu mmoja—ikiwa mwanadamu anaweza kusema kwa hakika kuwa ni kazi ya Mungu mmoja, basi dhana zake zitakuwa duni, na ambazo hazifai kutajwa. Kwa sababu maono ya mwanadamu hayako wazi, na mwanadamu anamjua tu Yehova kama Mungu, na Yesu kama Bwana, na ana mitazamo miwili kumhusu Mungu mwenye mwili wa leo, watu wengi wamejitoa kwa ajili ya kazi ya Yehova na Yesu, na wamezingirwa na dhana kuhusu kazi ya leo, watu wengi daima huwa na shaka na hawachukulii kazi ya leo kwa makini. Mwanadamu hana uelewa kuhusu hatua mbili za mwisho, ambazo hazikuonekana. Hio ni kwa sababu mwanadamu haelewi uhalisi wa hatua mbili za mwisho za kazi, na wala hakuzishuhudia binafsi. Ni kwa sababu haziwezi kuonekana ndiyo mwanadamu anawaza jinsi anavyopenda; bila kujali atakayodhanika, hakuna ukweli wa kudhibitisha, na yeyote wa kurekebisha. Mwanadamu anaruhusu silika yake ya asili itawale, huku akikosa kujali na kuachilia mawazo yake yaende popote, kwa kuwa hakuna ukweli wa kudhibitisha, na kwa hivyo dhana za mwanadamu zinakuwa “ukweli,” bila kujali kama zina dhibitisho. Kwa hivyo mwanadamu anaamini Mungu wake aliyemuwazia akilini mwake, na hamtafuti Mungu wa uhalisi. Ikiwa mtu mmoja ana aina moja ya imani, basi kati ya watu mia moja kuna aina mia moja za imani. Mwanadamu ana imani kama hizi kwa maana hajaona uhalisi wa kazi ya Mungu, kwa sababu amesikia tu kwa masikio yake na hajaona kwa macho yake. Mwanadamu amesikia hekaya na hadithi—lakini amesikia kwa nadra kuhusu maarifa ya ukweli ya kazi ya Mungu. Hivyo ni katika dhana zao ndivyo watu ambao wamekuwa waumini kwa mwaka mmoja tu wanaamini Mungu, na hilo ni kweli pia kwa wale ambao wamemwamini Mungu katika maisha yao yote. Wale ambao hawawezi kuona ukweli daima hawawezi kuepuka imani ambayo wana dhana kwazo kumhusu Mungu. Mwanadamu anaamini kuwa amejiweka huru kutokana na vifungo vya dhana zake za kale, na ameingia eneo jipya. Je, mwanadamu hajui kuwa maarifa ya wale wasioweza kuona uso wa kweli wa Mungu kuwa ni dhana na tetesi? Mwanadamu anafikiria kuwa dhana zake ni sawa, na wala hayana kasoro, na hufikiri kuwa hizi

dhana zimetoka kwa Mungu. Leo, mwanadamu anaposhuhudia kazi ya Mungu, anaachilia dhana zilizokuwa zimeongezeka kwa miaka mingi. Mawazo na dhana za awali zilikuwa vizuizi vya kazi ya hatua hii, na inakuwa vigumu kwa mwanadamu kuachana na dhana kama hizo na kupinga mawazo kama yale. Dhana kuhusu kazi hii ya hatua kwa hatua ya wengi wa wale wanaomfuata Mungu hadi leo zimekuwa za kuhuzunisha na watu hawa pole pole wamefanya uadui wa kikaidi na Mungu mwenye mwili hatua kwa hatua, na chanzo cha chuki ni mawazo na dhana za mwanadamu. Ni hasa kwa sababu ukweli haumruhusu mwanadamu kuwa na uhuru wa hiari ya mawazo yake, na, zaidi ya hayo, hauwezi kupingwa na mwanadamu kwa urahisi, na mawazo na dhana za mwanadamu hazistahimili uwepo wa ukweli, na hata zaidi ya hayo, kwa sababu mwanadamu hawezi kufikiria kuhusu usahihi na unyofu wa ukweli, na kwa nia moja tu huachilia mawazo yake, na hutumia dhana yake, kwamba dhana na mawazo ya mwanadamu zimekuwa adui wa kazi ya leo, kazi ambayo haiambatani na dhana za mwanadamu. Hili linaweza kusemwa kuwa kasoro ya dhana za mwanadamu, na wala si dosari ya kazi ya Mungu. Mwanadamu anaweza kufikiria lolote atakalo, lakini hawezi kupinga waziwazi hatua yoyote ya kazi ya Mungu au hata sehemu yoyote; ukweli wa kazi ya Mungu hauwezi kukiukwa na mwanadamu. Unaweza kuruhusu mawazo yako yatawale, na unaweza pia kujumuisha hadithi nzuri kuhusu kazi ya Yehova na Yesu, lakini kamwe huwezi kupinga ukweli wa kila hatua ya kazi ya Yehova na Yesu; hii ni kanuni, na pia ni amri ya utawala, na mnapaswa kuelewa umuhimu wa masuala haya. Mwanadamu anaamini kuwa hatua hii ya kazi hailingani na dhana za mwanadamu, na hivi sivyo katika hatua mbili zilizopita za kazi. Katika mawazo yake, mwanadamu anaamini kuwa kazi ya hatua mbili zilizopita kwa hakika si sawa na kazi ya leo—lakini je, umewahi kufikiria kuwa kanuni zote za kazi ya Mungu ni sawa, na kuwa kazi Yake huwa vitendo daima, na kuwa, bila kujali enzi, daima kutakuwa na halaiki ya watu wanaokataa na kuupinga ukweli wa kazi Yake? Wale wote ambao leo wanakataa na kuipinga hatua hii ya kazi bila shaka wangempinga Mungu wakati uliopita, kwa kuwa watu kama hawa daima watakuwa adui za Mungu. Watu wanaoujua ukweli wa kazi ya Mungu wataona hatua tatu za kazi kama kazi ya Mungu mmoja, na watatupilia mbali dhana zao. Hawa ni watu wanaomjua Mungu, na watu kama hawa ndio kwa kweli humfuata Mungu. Wakati ambapo usimamizi mzima wa Mungu utakaribia kufika mwisho, Mungu ataweka vitu vyote kulingana na aina. Mwanadamu aliumbwa kwa mikono ya Muumba, na mwishowe lazima kabisa Amrudishe mwanadamu chini ya utawala Wake; huu ndio mwisho wa hatua tatu za kazi. Hatua ya kazi ya siku za mwisho, na hatua mbili zilizopita katika Israeli na Yudea, ni mpango wa Mungu wa usimamizi katika dunia nzima. Hakuna anayeweza kupinga hili, na ni ukweli wa kazi ya Mungu. Ingawa watu hawajapata uzoefu ama kushuhudia nyingi za kazi hizi, ukweli unabaki kuwa ukweli, na hauwezi kukanwa na mwanadamu yeyote. Watu wanaomwamini Mungu katika nchi zote duniani watakubali hatua tatu za kazi. Kama wajua tu hatua moja ya kazi, na huelewi hatua nyingine

mbili za kazi, na huelewi kazi ya Mungu katika wakati uliopita, basi huwezi kuongea ukweli wa mpango mzima wa usimamizi wa Mungu, na maarifa yako ya Mungu yameegemea upande mmoja, kwa kuwa katika imani yako katika Mungu humfahamu, ama kumwelewa, na kwa hivyo hustahili kutoa ushuhuda wa Mungu. Bila kujali kama maarifa yako ya sasa ya mambo haya yana kina kirefu ama cha juujuu tu, mwishowe, lazima muwe na maarifa, na ushawishike kabisa, na watu wote wataona uzima wa kazi ya Mungu na kunyenyekea chini ya utawala wa Mungu. Mwishoni mwa kazi hii, madhehebu yote yatakuwa moja, viumbe wote watarejea chini ya utawala wa Muumba, viumbe wote watamwabudu Mungu mmoja wa kweli, na dini zote ovu zitakuwa bure, na hazitaonekana tena.

Mbona mfululizo huu wa marejeo kwa hatua tatu za kazi? Kupita kwa enzi, maendeleo ya kijamii, na uso wa asili unaobadilika yote hufuata mabadiliko katika hatua tatu za kazi. Mwanadamu hubadilika kwa wakati na kazi ya Mungu, na wala haku peke yake mwenyewe. Kutajwa kwa hatua tatu za kazi ya Mungu ni kwa ajili ya kuleta viumbe wote, na watu kutoka dini zote, chini ya utawala wa Mungu mmoja. Bila kujali wewe ni wa dini gani, mwishowe nyote mtanyenyekea chini ya utawala wa Mungu. Ni Mungu Mwenyewe tu anayeweza kufanya kazi hii; haiwezi kufanywa na kiongozi yeyote wa kidini. Kuna dini kadhaa kuu duniani, na kila moja ina kichwa, ama kiongozi, na wafuasi wameenea katika nchi tofauti na maeneo yote duniani; kila nchi, iwe ndogo au kubwa, ina dini tofauti ndani yake. Hata hivyo, bila kujali ni dini ngapi zilizo duniani, watu wote wanaoishi duniani mwishowe wanaishi katika uongozi wa Mungu mmoja, na uwepo wao hauongozwi na viongozi wa kidini au vichwa. Ambayo ni kusema kwamba wanadamu hawaongozwi na kiongozi fulani wa kidini ama kiongozi; badala yake wanadamu wote wanaongozwa na Muumba, aliyeziumba mbingu na nchi, na vitu vyote, na ambaye aliwaumba wanadamu—na huu ni ukweli. Hata ingawa dunia ina dini kadhaa kuu, bila kujali jinsi zilivyo kuu, zote zipo chini ya utawala wa Muumba, na hakuna inayoweza kuzidi wigo wa mamlaka hii. Maendeleo ya wanadamu, maendeleo ya kijamii, maendeleo ya sayansi ya asili—kila moja haitengani na mipango ya Muumba, na kazi hii sio kitu kinachoweza kufanywa na uongozi fulani wa dini. Viongozi wa dini ni viongozi tu wa dini fulani, na hawawezi kuwakilisha Mungu, ama Yule aliyeziumba mbingu na nchi na vitu vyote. Viongozi wa kidini wanaweza kuongoza wale wote walio katika dini yote, lakini hawawezi kuamrisha viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu—huu ni ukweli uliokubalika ulimwenguni. Viongozi wa dini ni viongozi tu, na hawawezi kuwa sawa na Mungu (Muumba). Vitu vyote vi mikononi mwa Muumba, na mwishowe vyote vitarejea mikononi mwa Muumba. Mwanadamu kiasili aliumbwa na Mungu, na haijalishi dini, kila mtu atarejea katika utawala wa Mungu—hili haliwezi kuepukika. Ni Mungu tu Aliye Juu Zaidi kati ya vitu vyote, na mtawala mkuu kati ya viumbe wote lazima pia warejee chini ya utawala Wake. Bila kujali mwanadamu ana hadhi ya juu kiasi gani, hawezi

kumfikisha mwanadamu kwenye hatima inayomfaa, wala hakuna anayeweza kuainisha kila kitu kulingana na aina. Yehova mwenyewe alimuumba mwanadamu na kumwainisha kila mmoja kulingana na aina na siku ya mwisho itakapowadia bado Atafanya kazi Yake Mwenyewe, kuanisha kila kitu kulingana na aina—hili haliwezi kufanywa na mwingine isipokuwa Mungu. Hatua tatu za kazi ambazo zilifanywa tangu mwanzo hadi leo zote zilitekelezwa na Mungu Mwenyewe, na zilitekelezwa na Mungu mmoja. Ukweli wa hatua tatu za kazi ni ukweli wa uongozi wa Mungu kwa wanadamu wote, ukweli ambao hakuna anayeweza kuupinga. Mwishoni mwa hatua tatu za kazi, vitu vyote vitaainishwa kulingana na aina na kurejea chini ya utawala wa Mungu, kwa kuwa duniani kote kuna Mungu mmoja tu, na hakuna dini nyingine. Yule asiyezeza kuiumba dunia hataweza kuiangamiza, ilhali Yule aliyeumba dunia hakika ataiangamiza, na kwa hivyo, kama mtu hana uwezo wa kutamatisha enzi na ni wa kumsaidia mwanadamu kukuza akili zake tu, basi hakika hatakuwa Mungu, na hakika hatakuwa Bwana wa mwanadamu. Hataweza kufanya kazi kuu kama hii; kuna mmoja tu anayeweza kufanya kazi kama hii, na wote wasioweza kufanya hii kazi hakika ni adui wala si Mungu. Dini zote ovu hazilingani na Mungu, na kwa sababu hawalingani na Mungu, wao ni adui za Mungu. Kazi yote inafanywa na huyu Mungu mmoja wa kweli, na ulimwengu mzima unatawaliwa na huyu Mungu mmoja. Bila kujali kama Anafanya kazi Uchina ama Israeli, bila kujali kama kazi inafanywa na Roho ama mwili, yote hufanywa na Mungu Mwenyewe, na haiwezi kufanywa na mwingine yeyote. Ni kabisa kwa sababu Yeye ni Mungu wa wanadamu wote ndiyo kwamba Yeye hufanya kazi kwa njia ya uhuru, pasipo kuwekewa masharti yoyote—na haya ndiyo maono makuu zaidi. Kama kiumbe wa Mungu, kama ungependa kutekeleza jukumu la kiumbe wa Mungu na kuelewa mapenzi ya Mungu, lazima uelewe kazi ya Mungu, lazima uelewe mapenzi ya Mungu kwa viumbe, lazima uelewe mpango Wake wa usimamizi, na lazima uelewe umuhimu wote wa kazi Anayofanya. Wale wasioelewa hivi hawajahitimu kuwa viumbe wa Mungu! Kama kiumbe wa Mungu, kama huelewi ulikotoka, huelewi historia ya mwanadamu na kazi yote iliyofanywa na Mungu, na, hata zaidi, huelewi jinsi mwanadamu ameendelea hadi leo, na huelewi ni nani anayeamuru wanadamu wote, basi huna uwezo wa kutekeleza wajibu wako. Mungu amemwongoza mwanadamu hadi leo, na tangu alipomuumba mwanadamu duniani Hajawahi kumwacha. Roho Mtakatifu daima haachi kufanya kazi, hajawahi kuacha kumwongoza mwanadamu, na hajawahi kumwacha. Lakini mwanadamu hatambui kuwa kuna Mungu, pia hamjui Mungu, na je, kuna jambo la kufedhehesha zaidi kuliko hili kwa viumbe wote wa Mungu? Mungu binafsi humwongoza mwanadamu, lakini mwanadamu haelewi kazi ya Mungu. Wewe ni kiumbe wa Mungu, ilhali huelewi historia yako mwenyewe, na wala hujui ni nani aliyekuongoza katika safari yako, hutambui kazi iliyofanywa na Mungu, na kwa hivyo huwezi kumjua Mungu. Ikiwa hujui sasa, basi hutawahi kuhitimu kutoa ushuhuda kwa Mungu. Leo, Muumba binafsi huwaongoza watu wote kwa mara nyingine, na kuwafanya watu wote kuona

hekima Yake, uweza, wokovu, na kustaajabisha Kwake. Ilhali bado hujatambua au kuelewa—na kwa hivyo, je, si wewe ndiwe utakayekosa kupokea wokovu? Wale walio wa Shetani hawaelewi maneno ya Mungu, na wale walio wa Mungu wanaweza kusikia sauti ya Mungu. Wale wote wanaotambua na kuelewa maneno Ninayozungumza ni wale watakaokolewa, na kumshuhudia Mungu; wote wasioelewa maneno Ninayoyazungumza hawawezi kutoa ushuhuda kwa Mungu, na ni wale watakaondolewa. Wale wasioyaelewa mapenzi ya Mungu na hawaitambui kazi ya Mungu hawawezi kupata maarifa ya Mungu, na watu kama hawa hawawezi kutoa ushuhuda kwa Mungu. Kama ungependa kumshuhudia Mungu, basi lazima umjue Mungu, na maarifa ya Mungu yanapatikana kwa kupitia kazi ya Mungu. Kwa ufupi, kama ungependa kumjua Mungu, basi lazima ujue kazi ya Mungu: Kufahamu kazi ya Mungu ndilo jambo la umuhimu kabisa. Hatua tatu za kazi zitakapofikia tamati, patafanyika kundi la watu wanaomshuhudia Mungu, kundi la wale wanaomjua Mungu. Watu hawa wote watamjua Mungu na wataweza kuonyesha ukweli kwa matendo. Watakuwa na ubinadamu na hisia, na wote watajua hatua tatu za kazi ya wokovu ya Mungu. Hii ndiyo kazi ambayo itatekelezwa mwishowe, na watu hawa ndio dhihirisho la kazi ya miaka 6,000 ya usimamizi, na ndio ushuhuda wenye nguvu zaidi kwa kushindwa kwa Shetani. Wale wanaoweza kumshuhudia Mungu wataweza kupokea ahadi na baraka za Mungu, na litakuwa ndilo kundi litakalosalia pale mwisho kabisa, lile linalomiliki mamlaka ya Mungu na lililo na ushuhuda wa Mungu. Pengine wale kati yenu wanaweza wote kuwa sehemu ya kundi hili, ama pengine nusu tu, ama wachache tu—inategemea radhi yenu na ufuatiliaji wenu.

Mwanadamu Aliyepotoka Anahitaji Zaidi Wokovu wa Mungu Mwenye Mwili

Mungu alifanyika mwili kwa sababu lengo la kazi Yake si roho ya Shetani, au kitu chochote kisicho cha mwili, ila mwanadamu, ambaye ni wa mwili na ambaye amepotoshwa na Shetani. Ni kwa sababu hii hasa kwamba mwili wa mwanadamu umepotoshwa ndiyo maana Mungu amemfanya mwanadamu mwenye mwili kuwa mlengwa wa kazi Yake; aidha, kwa sababu mwanadamu ni mlengwa wa upotovu, Amemfanya mwanadamu kuwa mlengwa wa pekee wa kazi Yake katika hatua zote za kazi Yake ya wokovu. Mwanadamu ni kiumbe anayekufa, ni wa mwili na damu, na Mungu ndiye tu Anayeweza kumwokoia mwanadamu. Kwa namna hii, ni lazima Mungu awe mwili ambao una tabia zinazofanana na mwanadamu ili Aweze kufanya kazi Yake, ili kwamba kazi Yake iweze kupata matokeo mazuri zaidi. Mungu lazima awe mwili ili Aweze kufanya kazi Yake kwa ufanisi kwa sababu mwanadamu ni wa mwili, na hana uwezo wa kushinda dhambi au kujivua mwili. Ingawa kiini na utambulisho wa Mungu unatofautiana kwa kiasi kikubwa na kiini na utambulisho wa mwanadamu, bado kuonekana Kwake kunafanana na

kuonekana kwa mwanadamu, Ana umbo la mwanadamu wa kawaida, na Anaishi maisha ya mwanadamu wa kawaida, na wale wanaomwona hawawezi kuona tofauti na mtu wa kawaida. Kuonekana huku kwa kawaida na ubinadamu wa kawaida vinatosha Kwake kwa ajili ya kufanya kazi Yake ya kiungu katika ubinadamu wa kawaida. Mwili Wake unamruhusu kufanya kazi Yake katika ubinadamu wa kawaida, na unamsaidia kufanya kazi Yake miongoni mwa wanadamu, na ubinadamu Wake wa kawaida, aidha, humsaidia kufanya kazi ya wokovu miongoni mwa wanadamu. Ingawa ubinadamu Wake wa kawaida umeleta msukosuko miongoni mwa wanadamu, msukosuko huo haujaathiri matokeo ya kawaida ya kazi Yake. Kwa ufupi, kazi ya ubinadamu Wake wa kawaida ni ya manufaa makubwa kwa mwanadamu. Ingawa watu wengi hawakubali ubinadamu Wake wa kawaida, kazi Yake bado inaweza kuwa ya ufanisi, na matokeo haya yanapatikana kutokana na ubinadamu Wake wa kawaida. Kuhusu hili hakuna shaka. Kutokana na kazi Yake ya mwili, mwanadamu anapata vitu mara kumi au dazeni kadhaa zaidi kuliko mitazamo iliyopo miongoni mwa mwanadamu kuhusu ubinadamu Wake wa kawaida, na mitazamo hiyo hatimaye itamezwa na kazi Yake. Na matokeo ambayo kazi Yake imefanikiwa, ambayo ni kusema, maarifa ambayo mwanadamu anayo juu Yake, yanazidi kwa mbali sana dhana za mwanadamu kumhusu. Hakuna namna ya kufikiri au kupima kazi Anayofanya katika mwili, maana mwili Wake si kama wa mwanadamu; ingawa sura za nje zinafanana kiini chao si sawa. Mwili Wake unatoa mitazamo mingi kuhusu Mungu miongoni mwa mwanadamu, bado mwili Wake unaweza pia kumruhusu mwanadamu kuwa na maarifa mengi, na anaweza hata kumshinda mwanadamu yeyote mwenye ganda la sawa nje. Maana Yeye si mwanadamu wa kawaida tu, bali ni Mungu mwenye umbo la nje kama la mwanadamu, na hakuna anayeweza kumwelewa au kumfahamu kikamilifu. Mungu asiyeonekana na kushikika anapendwa na kukaribishwa na wote. Kama Mungu ni Roho tu ambayo haionekani kwa mwanadamu, ni rahisi sana kwa mwanadamu kumwamini Mungu. Mwanadamu anaweza kuzipa uhuru fikra zake mwenyewe, anaweza kuchagua taswira yoyote anayotaka kama taswira ya Mungu ili kujifurahisha mwenyewe na kujifanya mwenyewe awe na furaha. Kwa njia hii, watu wanaweza kufanya yoyote yanayompendeza zaidi Mungu wao mwenyewe, na kile ambacho Mungu huyu angempenda wakifanye, bila aibu yoyote. Aidha, mwanadamu huyu anaamini kwamba hakuna ambaye ni mwaminifu zaidi anayejitolea kwa Mungu kuliko yeye, na kwamba wengine wote ni mbwa wa Mataifa, na wasiokuwa waaminifu kwa Mungu. Inaweza kusemekana kwamba hiki ndicho kinachotafutwa na wale ambao imani yao kwa Mungu ni ya kidhahania na ambayo imejikita katika mafundisho; wanavyovitafula vinafanana, tofauti ikiwa ndogo tu. Ni kwamba tu taswira za Mungu katika fikra zao ni tofauti, lakini viini vyao kimsingi vinafanana.

Mwanadamu hasumbuliwi na imani yake ya kutojali katika Mungu, na anamwamini Mungu kwa namna anavyotaka. Hii ni moja ya “haki na uhuru wa mwanadamu,” ambao hakuna mtu

anayeweza kuingilia kwa sababu mwanadamu anamwamini Mungu wake mwenyewe na wala si Mungu wa mtu yeyote yule; ni mali yake binafsi, na takribani kila mtu anamiliki aina hii ya mali binafsi. Mwanadamu anaichukulia mali hii kama hazina ya thamani, lakini kwa Mungu hakuna kitu ambacho ni duni au hakina thamani zaidi ya hiki, maana hakuna kiashiria cha wazi cha upinzani kwa Mungu kuliko mali hii binafsi ya mwanadamu. Ni kwa sababu ya kazi ya Mungu mwenye mwili ndiyo Mungu amefanyika mwili ambaye ana umbo la kugusika, na ambaye anaweza kuonekana na kuguswa na mwanadamu. Yeye si Roho asiyekuwa na umbo, bali mwili ambao unaweza kuhusiana na kuonekana kwa mwanadamu. Hata hivyo, Miungu mingi ambayo watu wanaamini kwayo ni miungu isiyo na mwili na umbo maalumu, na ambayo haifungwi na umbo maalumu. Kwa njia hii, Mungu mwenye mwili amekuwa adui wa wengi wanaomwamini Mungu, na wale ambao hawawezi kuukubali ukweli wa Mungu mwenye mwili, vilevile, wamekuwa maadui wa Mungu. Mwanadamu amejawa na dhana si kwa sababu ya namna anavyofikiri, au kwa sababu ya uasi wake, bali ni kwa sababu ya mali hii binafsi ya mwanadamu. Ni kwa sababu ya mali hii watu wengi hufa, na ni Mungu huyu asiye dhahiri, ambaye hawezi kuguswa, hawezi kuonwa, na ambaye hayupo hakika ambaye huangamiza maisha ya mwanadamu. Maisha ya mwanadamu yanapotea si kwa sababu ya Mungu mwenye mwili, sembuse na Mungu wa mbinguni, bali ni Mungu wa fikra za mwanadamu mwenyewe. Sababu pekee ambayo Mungu mwenye mwili amefanyika mwili ni kwa sababu ya mahitaji ya mwanadamu aliyepotoka. Ni kwa sababu ya mahitaji ya mwanadamu na si ya Mungu, na mateso Yake na sadaka ni kwa ajili ya mwanadamu na si kwa manufaa ya Mungu Mwenyewe. Hakuna faida wala hasara au tuzo kwa Mungu; Hatavuna mavuno yoyote ya baadaye, bali ni kile ambacho hapo awali Aliwiwa. Yote Anayoyafanya na kujitolea kwa ajili mwanadamu si kwa sababu Atapata thawabu kubwa, bali ni kwa ajili ya mwanadamu. Ingawa kazi ya Mungu mwenye mwili inahusisha ugumu mwingi usiofikirika, matokeo ambayo yanapatikana mwishowe yanazidi kwa mbali sana kazi inayofanywa na Roho Mtakatifu moja kwa moja. Kazi ya mwili inahusisha taabu nyingi sana, na mwili hauwezi kuwa na utambulisho mkubwa kama wa Roho, hauwezi kufanya matendo ya kimiujiza kama Roho, sembuse kuwa na mamlaka kama ya Roho. Lakini kiini cha kazi inayofanywa na mwili huu usiokuwa wa kawaida ni kuu zaidi kulinganisha na kazi inayofanywa moja kwa moja na Roho, na mwili huu Mwenyewe ndio jibu kwa mahitaji yote ya wanadamu wote. Kwa wale wanaotaka kuokolewa, thamani ya Roho ipo chini zaidi kulinganisha na ile ya mwili. Kazi ya Roho inaweza kuufikia ulimwengu wote, katika milima yote, mito, maziwa, na bahari, lakini kazi ya mwili kwa ufanisi zaidi inahusiana na kila mtu anayekutana na Yeye. Aidha, mwili wa Mungu katika umbo la kushikika unaweza kueleweka vizuri na kuaminiwa na mwanadamu, na unaweza kuimarisha maarifa ya mwanadamu kuhusu Mungu, na anaweza kumwachia mwanadamu mvuto wa kina wa matendo halisi ya Mungu. Kazi ya Roho imefungwa sirini, ni vigumu kwa viumbe wenye mwili wa kufa

kuelewa, na vigumu zaidi kwao kuona, na hivyo wanaweza kutegemea tu vitu vya kufikirika. Hata hivyo, kazi ya mwili ni ya kawaida, na imejikita katika uhalisi, na ina hekima kubwa sana, na ni ukweli unaoweza kuonekana kwa macho ya mwanadamu; mwanadamu anaweza kupitia uzoefu wa hekima ya Mungu, na hana haja ya kuwa na fikira zake kubwa. Huu ndio usahihi na thamani halisi ya kazi ya Mungu mwenye mwili. Roho anaweza tu kufanya vitu ambavyo havionekani kwa mwanadamu na vigumu kwake kufikiria, kwa mfano nuru ya Roho, mzunguko wa Roho na uongozi wa Roho, lakini kwa mwanadamu mwenye akili, hivi havitoi maana inayoeleweka. Vinatoa maana ya kusonga, au ya jumla tu, na havitoi maelekezo kwa maneno. Hata hivyo, kazi ya Mungu mwenye mwili, ni tofauti sana: Ina mwongozo sahihi wa maneno, ina nia ya wazi, ina malengo ya wazi yanayohitajika. Na hivyo mwanadamu hahitaji kupapasa, au kutumia fikra zake, au kufanya makisio. Huu ndio uwazi wa kazi katika mwili, na tofauti yake kubwa na kazi ya Roho. Kazi ya Roho inafaa tu kwa mawanda finyu, na haiwezi kuchukua kazi ya mwili. Kazi ya mwili inampa mwanadamu malengo halisi zaidi na yanayohitajika na maarifa yaliyo halisi zaidi na yenye thamani kuliko kazi ya Roho Mtakatifu. Kazi ambayo ina thamani kubwa kwa mwanadamu aliyepotoka ambayo inatoa maneno sahihi, malengo wazi ya kufuata, na ambayo inaweza kuonekana na kuguswa. Ni kazi yenye kuwezekana tu, na uongozi wa wakati ndio unaofaa kwa ladha ya mwanadamu, na kazi halisi ndiyo inayoweza kumwokoza mwanadamu kutoka katika tabia yake iliyopotoka na kusawijika. Hii inaweza kufanywa na Mungu mwenye mwili tu; ni Mungu mwenye mwili peke yake ndiye Anayeweza kumwokoza mwanadamu kutoka katika hali yake ya zamani ya kupotoka. Ingawa Roho ni kiini cha asili ya Mungu, kazi kama hii inaweza tu kufanywa na mwili Wake. Kama Roho angefanya kazi peke Yake, basi haingewezekana kwa kazi Yake kuwa ya ufanisi—huu ni ukweli ulio wazi kabisa. Ingawa watu wengi wamekuwa maadui wa Mungu kwa sababu ya mwili huu, Anapokamilisha kazi Yake, wale ambao wapo kinyume Chake hawataacha tu kuwa maadui Zake, bali kinyume Chake watakuwa mashahidi Wake. Watakuwa mashahidi watakaokuwa wameshindwa naye, mashahidi ambao wana ulinganifu na Yeye na ambao hawatenganishwi naye. Atamsababisha mwanadamu kujua umuhimu wa kazi Yake katika mwili kwa mwanadamu, na mwanadamu atajua umuhimu wa mwili huu katika maana ya uwepo wa mwanadamu, atajua thamani Yake halisi katika ukuaji wa maisha ya mwanadamu, aidha, atajua mwili huu utakuwa chemchemi ya uhai ambayo kwayo mwanadamu hataachana nayo. Ingawa Mungu mwenye mwili anatofautiana sana na utambulisho na nafasi ya Mungu, na anaonekana kwa mwanadamu kuwa hana ulinganifu na hadhi yake halisi, mwili huu, ambao hauna sura halisi ya Mungu, au utambulisho halisi wa Mungu, unaweza kufanya kazi ambayo Roho wa Mungu hawezi kuifanya moja kwa moja. Hiyo ndiyo maana ya kweli na thamani ya Mungu mwenye mwili, na ni umuhimu huu na thamani ambayo mwanadamu hawezi kuithamini na kuikubali. Ingawa wanadamu wote wanamtazamia Roho wa Mungu na wanamdharau Mungu mwenye mwili, bila kujali vile wanavyoona au kufikiri, maana

na thamani halisi ya mwili inapita kwa mbali ile ya Roho. Bila shaka, hii ni kwa mujibu wa mwanadamu aliyepotoka. Kwa kuwa kila mtu anayetafuta ukweli na anatamani kumwona Mungu, Kazi ya Roho inaweza kutoa tu kuguswa au msukumo, na hisia ya kuona maajabu ambayo hayaelezeki na kufikirika, na hisia ambayo ni kuu, ya juu sana kuliko uwezo wa mwanadamu, na inayotamanika, lakini ambayo pia haifikiwi na haipatikani kwa wote. Mwanadamu na Roho wa Mungu wanaweza tu kutazamana kwa mbali, kana kwamba kuna umbali mrefu baina yao, na hawawezi kufanana kamwe, kana kwamba mwanadamu na Mungu wametenganishwa na mgawanyiko usioonekana. Kwa hakika, hizi ni fikra za uongo ambazo Roho amempa mwanadamu, ambayo ndiyo sababu Roho na mwanadamu sio wa aina moja, na Roho na mwanadamu hawawezi kuishi pamoja katika ulimwengu mmoja, na kwa sababu Roho hana kitu chochote cha mwanadamu. Kwa hivyo mwanadamu hana haja ya Roho, maana Roho hawezi kufanya kazi inayohitajika sana na mwanadamu moja kwa moja. Kazi ya mwili inampatia mwanadamu malengo halisi ya kufuata, maneno halisi, na hisia kwamba Yeye ni halisi na wa kawaida, kwamba ni mnyenyekevu na wa kawaida. Ingawa mwanadamu anaweza kumwogopa, kwa watu wengi Yeye ni rahisi kuhusiana naye: Mwanadamu anaweza kuuona uso Wake, na kuisikia sauti Yake, na hahitaji kumwangalia kwa kutokea mbali. Mwanadamu anahisi kuwa ni rahisi kuufikia mwili huu, sio wa mbali au usioeleweka, bali unaoonekana na kushikika, maana mwili huu upo katika ulimwengu mmoja na mwanadamu.

Kwa wale wote ambao wanaishi katika mwili, kubadilisha tabia zao kunahitaji kuwe na malengo ya kufuata, na kumjua Mungu kunahitaji kushuhudia matendo halisi na sura halisi ya Mungu. Yote haya yanaweza kufikiwa tu na Mungu mwenye mwili, na yote yanaweza kukamilishwa na mwili wa kawaida na halisi. Hii ndiyo maana kufanyika mwili ni muhimu, na kwa nini kunahitajika na wanadamu wote wapotovu. Kwa kuwa watu wanahitajika kumjua Mungu, taswira za Mungu wa kufikirika na wa kimiujiza inapaswa iondolewe kutoka katika mioyo yao, na kwa kuwa wanahitajika kutupilia mbali tabia yao iliyopotoka, kwanza wanapaswa kujua tabia yao iliyopotoka. Ikiwa mwanadamu anafanya kazi ili kuondoa taswira za Miungu wasio dhahiri kutoka katika mioyo ya watu, basi atashindwa kupata matokeo sahihi. Taswira za Miungu wasio dhahiri katika mioyo ya watu haziwezi kuwekwa hadharani, kutupwa, au kufukuzwa kabisa kwa maneno pekee. Kwa kufanya hivyo, mwisho wake haitawezekana kuondoa vitu hivi vilivyokita mizizi kwa watu. Ni kwa kubadilisha vitu hivi visivyo dhahiri na vya kimiujiza na Mungu anayeonekana tu na mwenye taswira halisi ya Mungu, na kuwafanya watu kuvielewa ndipo matokeo mazuri yanaweza kupatikana. Mwanadamu anatambua kwamba Mungu aliyekuwa anamtafuta huko nyuma ni asiye dhahiri na wa kimiujiza. Kile ambacho kinaweza kufanikisha matokeo haya sio uongozi wa moja kwa moja wa Roho, sembuse mafundisho ya mtu fulani, bali ni Mungu mwenye mwili. Dhana za mwanadamu zinakuwa wazi

pale ambapo Mungu mwenye mwili atafanya kazi Yake rasmi, kwa sababu ukawaida na uhalisi wa Mungu mwenye mwili ni kinyume na nadharia za Mungu asiye dhahiri na wa kufikirika katika fikra za mwanadamu. Dhana asili za mwanadamu zinaweza tu kudhihirishwa kupitia tofauti zao na Mungu mwenye mwili. Bila ulinganisho na Mungu mwenye mwili, dhana za mwanadamu zisingefichuliwa; kwa maneno mengine, bila tofauti ya uhalisi vitu visivyo dhahiri visingefichuliwa. Hakuna anayeweza kutumia maneno ili kufanya kazi hii, na hakuna anayeweza kuizungumzia kazi hii kwa kutumia maneno. Ni Mungu Mwenyewe pekee ndiye Anayeweza kufanya kazi Yake, na hakuna mtu mwingine anayeweza kufanya kazi hii kwa niaba Yake. Haijalishi lugha ya mwanadamu ni pevu kiasi gani, hawezi kuzungumzia uhalisi na ukawaida wa Mungu. Mwanadamu anaweza tu kumjua Mungu zaidi kwa utendaji, na anaweza tu kumwona kwa uwazi zaidi, ikiwa Mungu binafsi anafanya kazi miongoni mwanadamu na anaonyesha kikamilifu sura Yake na uungu Wake. Athari hii haiwezi kupatwa na mwanadamu yeyote yule mwenye mwili. Bila shaka, Roho wa Mungu pia hawezi kupata matokeo haya. Mungu anaweza kumwokoza mwanadamu kutoka katika ushawishi wa Shetani, lakini kazi hii haiwezi kukamilishwa moja kwa moja na Roho wa Mungu; badala yake, inaweza kufanywa tu na mwili ambao Roho wa Mungu anauvaa, na mwili wa Mungu mwenye mwili. Mwili huu ni mwanadamu na pia ni Mungu, ni mwanadamu aliye katika ubinadamu wa kawaida na pia ni Mungu ambaye ana uungu wote. Na hivyo, hata kama mwili huu sio Roho wa Mungu, na unatofautiana kwa kiasi kikubwa na Roho, bado ni Mungu mwenye mwili Mwenyewe ambaye Anamwokoza mwanadamu, ambaye ni Roho, pia ni mwili. Haijalishi Anaitwa majina gani, hatimaye bado ni Mungu Mwenyewe anayemwokoza mwanadamu. Maana Roho wa Mungu hatenganishwi na mwili, na kazi ya mwili pia ni kazi ya Roho wa Mungu; ni kwamba tu kazi hii haifanywi kwa kutumia utambulisho wa Roho, lakini inafanywa kwa kutumia utambulisho wa mwili. Kazi inayotakiwa kufanywa moja kwa moja na Roho haihitaji kufanyika mwili, na kazi ambayo inahitaji mwili kuifanya haiwezi kufanywa moja kwa moja na Roho, na inaweza kufanywa tu na Mungu mwenye mwili. Hiki ndicho kinachohitajika kwa kazi hii, na ndicho kinachohitajika na mwanadamu aliyepotoka. Katika hatua tatu za kazi ya Mungu, ni hatua moja tu ndiyo iliyofanywa moja kwa moja na Roho, na hatua mbili zilizobaki zimechukuliwa na Mungu mwenye mwili, na hazifanywi moja kwa moja na Roho. Kazi ya Enzi ya Sheria iliyofanywa na Roho haikuhusisha kubadilisha tabia potovu ya mwanadamu, na wala haikuwa na uhusiano wowote na maarifa ya mwanadamu kuhusu Mungu. Hata hivyo kazi ya Mungu mwenye mwili katika Enzi ya Neema na Enzi ya Ufalme, inahusisha tabia ya dhambi ya mwanadamu na maarifa yake juu ya Mungu, na ni sehemu ya maana na muhimu ya kazi ya wokovu. Kwa hiyo, mwanadamu aliyepotoka anahitaji zaidi wokovu wa Mungu mwenye mwili, na anahitaji zaidi kazi ya moja kwa moja ya Mungu mwenye mwili. Mwanadamu anahitaji Mungu mwenye mwili ili kumchungu, kumsaidia, kumnywesha maji, kumlisha, kumhukumu na

kumwadibu, na anahitaji neema zaidi na wokovu mkubwa kutoka kwa Mungu mwenye mwili. Ni Mungu katika mwili pekee ndiye anayeweza kuwa msiri wa mwanadamu, mchungaji wa mwanadamu, msaada wa mwanadamu uliopo kila mara, na hii yote ni ulazima wa kufanyika mwili leo na katika nyakati za nyuma.

Mwanadamu amepotoshwa na Shetani, na yeye ndiye kiumbe wa juu kabisa kuliko viumbe wote wa Mungu, hivyo mwanadamu anahitaji wokovu wa Mungu. Mlengwa wa wokovu wa Mungu ni mwanadamu, si Shetani, na kile kitakachookolewa ni mwili wa mwanadamu, na roho ya mwanadamu, na si mwovu. Shetani ni mlengwa wa uharibifu wa Mungu, mwanadamu ni mlengwa wa wokovu wa Mungu, na mwili wa mwanadamu umepotoshwa na Shetani, kwa hivyo kitu cha kwanza kuokolewa ni mwili wa mwanadamu. Mwili wa mwanadamu umepotoshwa kwa kiasi kikubwa, na umekuwa kitu cha kumpinga Mungu, ambacho kinapinga na kukana waziwazi uwepo wa Mungu. Mwili huu uliopotoka ni vigumu sana kushughulika nao, na hakuna kitu ambacho ni kigumu sana kushughulika nacho au kukibadilisha kuliko tabia potovu ya mwili. Shetani anaingia katika mwili wa mwanadamu ili kuchochea usumbufu, na anatomia mwili wa mwanadamu kuisumbua kazi ya Mungu, na kuharibu mpango wa Mungu, na hivyo mwanadamu amekuwa Shetani, na adui wa Mungu. Ili mwanadamu aweze kuokolewa, kwanza ni lazima achukuliwe mateka. Ni kwa sababu hii ndiyo maana Mungu anainuka na kuingia katika vita na Anaingia katika mwili ili afanye kazi ambayo Amekusudia kufanya, na kupambana na Shetani. Lengo Lake ni wokovu wa mwanadamu, mwanadamu ambaye amepotoshwa, na kushindwa na kuangamizwa kwa Shetani, ambaye ameasi dhidi Yake. Anamshinda Shetani kupitia kazi Yake ya kumshinda mwanadamu, na huku akimwoko mwanadamu aliyepotoka. Hivyo, ni kazi ambayo inatimiza matatizo mawili kwa wakati mmoja. Anafanya kazi makusudi mawili mwili mara moja na Anazungumza katika mwili, na Anafanya kazi zote katika mwili ili aweze kujihusisha vizuri na mwanadamu, na kumdhibiti mwanadamu vizuri. Wakati wa mwisho ambapo Mungu atakuwa mwili, kazi Yake katika siku za mwisho itahitimishwa katika mwili. Atawaainisha wanadamu wote kulingana na aina, na kuhitimisha usimamizi wake wote, na pia kuhitimisha kazi Yake yote katika mwili. Baada ya kazi Yake yote duniani kuisha, Atakuwa mshindi kikamilifu. Kufanya kazi katika mwili, Mungu atakuwa amemshinda mwanadamu kikamilifu na atakuwa amempata mwanadamu kikamilifu. Hii haimaanishi kuwa usimamizi Wake wote utakuwa umekoma? Mungu anapohitimisha kazi Yake katika mwili, ilivyo kwamba Amemshinda Shetani kikamilifu, na Amekuwa mshindi, Shetani hatakuwa na fursa zaidi ya kumpotosha mwanadamu. Kazi ya Mungu mwenye mwili wa kwanza ilikuwa ni wokovu na msamaha wa dhambi za mwanadamu. Sasa ni kazi ya kumshinda na kumpata mwanadamu, ili kwamba Shetani asiweze tena kufanya kazi yake, na atakuwa amepotea kabisa, na Mungu atakuwa ameshinda kabisa. Hii ni kazi ya mwili, na ni kazi inayofanywa na Mungu Mwenyewe.

Kazi ya awali ya hatua tatu za kazi ya Mungu ilifanywa moja kwa moja na Roho, na wala si mwili. Hata hivyo, kazi ya mwisho ya hatua tatu za kazi ya Mungu, inafanywa na Mungu mwenye mwili, na wala haifanywi moja kwa moja na Roho. Kazi ya ukombozi ya hatua ya katikati pia imefanywa na Mungu mwenye mwili. Katika kazi yote ya usimamizi, kazi muhimu sana ni wokovu kutoka katika ushawishi wa Shetani. Kazi muhimu ni kumshinda kabisa mwanadamu aliyepotoka, na hivyo kurejesha heshima ya awali ya Mungu katika moyo wa mwanadamu, na kumruhusu kufikia maisha ya kawaida, ni sawa na kusema, maisha ya kawaida ya kiumbe wa Mungu. Kazi hii ni muhimu, na ni kiini cha kazi ya usimamizi. Katika hatua tatu za kazi ya wokovu, hatua ya kwanza ya kazi ya Enzi ya Sheria inatofautiana sana na kiini cha kazi ya usimamizi; ilikuwa tu ina kuonekana kwa mbali kwa kazi ya wokovu, na haikuwa mwanzo wa kazi ya Mungu ya kumwokoa mwanadamu kutoka katika utawala wa Shetani. Hatua ya kwanza ya kazi ilifanywa na Roho kwa sababu, chini ya sheria, mwanadamu alijua tu kuzishika sheria, na hakuwa na ukweli zaidi, na kwa sababu kazi katika Enzi ya Sheria haikujihusisha na kubadilisha tabia ya mwanadamu, sembuse haikuwa inajihusisha na kazi ya jinsi ya kumwokoa mwanadamu kutoka katika utawala wa Shetani. Roho wa Mungu alikamilisha hatua hii rahisi ya kazi ambayo haikujihusisha na tabia iliyopotoka ya mwanadamu. Hatua hii ya kazi ilikuwa na uhusiano mdogo na kiini cha usimamizi na haikuwa na uhusiano mkubwa na kazi rasmi ya wokovu wa mwanadamu, na kwa hivyo haikumhitaji Mungu ili aweze kuifanya kazi Yake. Kazi inayofanywa na Roho ni dhahiri na haifahamiki, na ya kutisha kwa kina isiyofikiwa kwa mwanadamu; Roho hafai kikamilifu kwa ajili ya kufanya kazi ya wokovu moja kwa moja, na hafai kikamilifu kwa ajili ya kumpa mwanadamu uzima moja kwa moja. Kinachomfaa zaidi mwanadamu ni kubadilisha kazi ya Roho na kuwa katika hali ambayo inamkaribia mwanadamu, yaani, kile kinachomfaa mwanadamu zaidi ni Mungu kuwa mtu wa kawaida ili kufanya kazi Yake. Hili linahitaji Mungu apate mwili ili kuchukua kazi ya Roho, na kwa mwanadamu, hakuna njia inayofaa zaidi ya Mungu kufanya kazi. Kati ya hatua hizi tatu za kazi, hatua mbili zinafanywa na mwili, na hatua hizi mbili ni awamu muhimu ya kazi ya usimamizi. Kupata mwili huku kuwili kunakamilishana na kuafikiana. Hatua ya kwanza ya Mungu mwenye mwili iliweka msingi kwa ajili ya hatua ya pili, na tunaweza kusema kwamba kupata mwili huku kuwili kwa Mungu kunafanya hatua moja, na zote hazina ulinganifu. Hatua mbili hizi za kazi ya Mungu zinafanywa na Mungu katika utambulisho Wake katika mwili kwa sababu zina umuhimu sana katika kazi nzima ya usimamizi. Inaweza kusemwa kuwa, bila kazi ya Mungu mwenye mwili katika hatua mbili hizi, kazi nzima ya usimamizi ingefikia kikomo kwa ghafla, na kazi ya kumwokoa mwanadamu isingekuwa kitu isipokuwa maneno matupu. Haijalishi kazi hii ni muhimu au si muhimu lakini imejikita katika mahitaji ya mwanadamu, na uhalisi wa upotovu wa mwanadamu, na uzito wa kutotii kwa Shetani na usumbufu wake katika kazi. Mhusika sahihi ni yule anayeifanya kazi ametabiriwa na asili ya kazi inayofanywa na huyo

mfanyakazi, na umuhimu wa kazi. Unapokuja umuhimu wa kazi hii, kwa misingi ya mbinu ya kutumia—kazi inayofanywa moja kwa moja na Roho wa Mungu, au kazi inayofanywa na Mungu mwenye mwili, au kazi inayofanywa kupitia mwanadamu—ya kwanza kuondolewa ni kazi inayofanywa kupitia mwanadamu, na kulingana na asili ya kazi, na asili ya kazi ya Roho dhidi ya ile ya mwili, hatimaye inaamuliwa kwamba kazi inayofanywa na mwili ni ya manufaa zaidi kwa mwanadamu kuliko kazi inayofanywa moja kwa moja na Roho, na inakuwa na manufaa zaidi. Hili ni wazo la Mungu wakati wa kuamua ama kazi ifanywe na Roho au ifanywe na mwili. Kuna umuhimu na msingi katika kila hatua ya kazi. Siyo fikra tu zisizo na msingi, na wala hazifanywi kiholela; kuna hekima fulani ndani yake. Huo ndio ukweli wa kazi zote za Mungu. Hasa, kuna mpango wa Mungu zaidi katika kazi kubwa kama hiyo kwa kuwa Mungu mwenye mwili akifanya kazi miongoni mwa wanadamu. Na kwa hivyo, hekima ya Mungu na uungu Wake wote unaakisiwa katika kila tendo Lake, fikira, na wazo katika kufanya kazi; huu ndio uungu wa Mungu ambao uko imara na wenye mpangilio. Fikira hizi na mawazo ya kutatiza ni ngumu kwa mwanadamu kuwaza, na mambo magumu kwa mwanadamu kuamini, aidha, magumu kwa mwanadamu kuyafahamu. Kazi inayofanywa na mwanadamu ni kulingana na kanuni ya ujumla, ambayo, kwa mwanadamu, ni ya kuridhisha sana. Lakini ikilinganisha na kazi ya Mungu, kuna tofauti kubwa sana; ingawa matendo ya Mungu ni makuu na kazi ya Mungu ni ya kiwango cha juu sana, nyuma yake kuna mipango na mipangilio midogo ya uhakika ambayo haiwezi kufikirika kwa mwanadamu. Kila hatua ya kazi Yake sio kulingana na kanuni tu, lakini pia inajumuisha vitu vingi ambavyo haviwezi kusemwa kwa lugha ya kibinadamu, na haya ni mambo ambayo hayaonekani kwa mwanadamu. Bila kujali kama ni kazi ya Roho au kazi ya Mungu mwenye mwili, kila kazi inajumuisha mpango wa kazi Yake. Hafanyi kazi bila kuwa na msingi, na hafanyi kazi isiyokuwa na maana. Roho anapofanya kazi moja kwa moja, ni kwa malengo Yake, na Anapokuwa mwanadamu (ambayo ni sawa na kusema, Anapobadilisha ganda Lake la nje) kufanya kazi, ni zaidi hata na lengo Lake. Kwa sababu ipi nyingine kwa urahisi Abadilishe utambulisho Wake vivi hivi tu? Kwa sababu ipi nyingine kwa urahisi Abadilike awe mtu ambaye anachukuliwa kuwa ni duni na kuteswa?

Kazi Yake katika mwili ni ya umuhimu mkubwa, ambao umezungumzwa kuhusiana na kazi, na Yule ambaye hatimaye anahitimisha kazi ni Mungu mwenye mwili, na sio Roho. Baadhi ya watu wanaamini kwamba Mungu wakati fulani anaweza kuja duniani na kumtokea mwanadamu, ambapo Atawahukumu wanadamu wote, akimjaribu mmoja baada ya mwingine bila mtu yeyote kupitwa. Wale wanaofikiri kwa namna hii hawafahamu hatua hii ya kazi ya Mungu mwenye mwili. Mungu hamhukumu mwanadamu mmoja baada ya mwingine, na hamjaribu mwanadamu mmoja baada ya mwingine; kufanya hivyo hakungekuwa kazi ya hukumu. Je, upotovu wa wanadamu wote si ni sawa? Je, kiini cha wanadamu wote hakifanani?

Kinachohukumiwa ni kiini cha mwanadamu kilichopotoka, kiini cha mwanadamu kilichopotoshwa na Shetani, na dhambi zote za mwanadamu. Mungu hahukumu makosa madogo madogo ya mwanadamu na yasiyokuwa na umuhimu. Kazi ya hukumu ni ya uwakilishi, na haifanywi mahususi kwa ajili ya mtu fulani. Badala yake, ni kazi ambayo kwayo kundi la watu wanahukumiwa ili kuiwakilisha hukumu ya wanadamu wote. Kwa Yeye mwenyewe kufanya kazi Yake katika kundi la watu, Mungu mwenye mwili anatumia kazi Yake ili kuwakilisha kazi ya wanadamu wote, ambayo inaenea taratibu. Kazi ya hukumu pia iko hivyo. Mungu hahukumu aina fulani ya mtu au kundi fulani la watu, bali anawahukumu wasio na haki wote miongoni mwa wanadamu—upinzani wa mwanadamu kwa Mungu, kwa mfano, au mwanadamu kutomcha Yeye, au kusababisha usumbufu katika kazi ya Mungu, na kadhalika. Kile kinachohukumiwa ni kiini cha mwanadamu cha kumpinga Mungu, na kazi hii ni kazi ya ushindi ya siku za mwisho. Kazi na neno la Mungu mwenye mwili lililoshuhudiwa na mwanadamu ni kazi ya hukumu mbele ya kiti kikuu cheupe cha enzi wakati wa siku za mwisho, ambacho kilibuniwa na mwanadamu katika kipindi cha siku za nyuma. Kazi ambayo sasa inafanywa na Mungu mwenye mwili ni hukumu yenyewe mbele ya kiti kikuu cheupe cha enzi. Mungu mwenye mwili wa leo ni Yule Mungu anayewahukumu wanadamu wote wakati wa siku za mwisho. Mwili huu na kazi, neno, na tabia Yake yote, vyote ni ujumla Wake. Ingawa mawanda ya kazi Yake ni finyu, na hayahusishi moja kwa moja ulimwengu wote, kiini cha kazi ya hukumu ni hukumu ya moja kwa moja kwa wanadamu wote; si kazi inayofanywa kwa ajili ya watu weteule Uchina tu, au kwa ajili ya idadi ndogo ya watu. Wakati wa kazi ya Mungu mwenye mwili, ingawa mawanda ya kazi hii hayahusishi ulimwengu mzima, inawakilisha kazi ya ulimwengu mzima na, baada ya kuhitimisha kazi ndani ya mawanda ya mwili Wake, Ataipanua kazi hii mara moja katika ulimwengu mzima, kwa namna ile ile, injili ya Yesu ilienea ulimwengu mzima baada ya kufufuka Kwake na kupaa mbinguni. Bila kujali endapo ni kazi ya Roho au ni kazi ya mwili, ni kazi ambayo inafanywa ndani ya mawanda finyu, lakini ambayo inauwakilisha ulimwengu mzima. Wakati wa siku za mwisho, Mungu anaonekana kufanya kazi Yake kwa kutumia utambulisho Wake wa Mungu mwenye mwili, na Mungu mwenye mwili ni Mungu anayemhukumu mwanadamu mbele ya kiti kikuu cheupe cha enzi. Bila kujali endapo ni Roho au mwili, Yule ambaye anafanya kazi ya hukumu ni Mungu anayemhukumu mwanadamu katika siku za mwisho. Hii inafasiliwa kwa kutegemeza kwa kazi Yake, na haifasiliwi kulingana na umbo Lake la nje au sababu nyinginezo. Ingawa mwanadamu ana dhana za maneno haya, hakuna anayeweza kukana ukweli wa hukumu ya Mungu mwenye mwili na kuwashinda wanadamu wote. Bila kujali ni jinsi gani binadamu anafikiri kuuhusu, ukweli ni, baada ya yote, ukweli tu. Hukuna anayeweza kusema “Kazi imefanywa na Mungu lakini mwili si Mungu.” Huu ni upuuzi, maana kazi hii haiwezi kufanywa na mtu yeyote isipokuwa Mungu mwenye mwili. Kwa kuwa kazi hii imekwishakamilika, kufuatia kazi hii, kazi ya hukumu ya Mungu kwa

mwanadamu haitatokea kwa mara ya pili; Mungu katika kupata mwili Kwake mara ya pili amekwishaikamilisha kazi yote ya usimamizi, na hakutakuwa na hatua ya nne ya kazi ya Mungu. Kwa sababu yule anayehukumiwa ni mwanadamu, mwanadamu ambaye ni wa mwili na ambaye amepotoshwa, na sio roho ya Shetani ambayo inahukumiwa moja kwa moja, kazi ya hukumu haifanywi katika ulimwengu wa roho, bali miongoni mwa wanadamu. Hakuna anayefaa zaidi na anayestahili, kuliko Mungu mwenye mwili kwa ajili ya kuhukumu upotovu wa mwili wa mwanadamu. Ikiwa hukumu ingefanywa moja kwa moja na Roho wa Mungu, basi isingekuwa inajumuisha wote. Aidha, kazi kama hiyo itakuwa vigumu kwa mwanadamu kuikubali, maana Roho hawezi kukutana uso kwa uso na mwanadamu, na kwa sababu hii, matokeo hayawezi kuwa ya haraka, sembuse mwanadamu hataweza kuona kwa uwazi kabisa tabia ya Mungu isiyokosewa. Shetani anaweza tu kushindwa kabisa ikiwa Mungu mwenye mwili anahukumu upotovu wa mwanadamu. Kuwa sawa na mwanadamu akiwa na ubinadamu wa kawaida, Mungu mwenye mwili anaweza kumhukumu mwanadamu asiye na haki; hii ni ishara ya utakatifu Wake wa ndani na hali Yake ya kutokuwa wa kawaida. Ni Mungu pekee ndiye anayestahili, na aliye katika nafasi ya kumhukumu mwanadamu, maana Ana ukweli, na mwenye haki, na kwa hivyo Ana uwezo wa kumhukumu mwanadamu. Wale ambao hawana ukweli na haki hawafai kuwahukumu wengine. Ikiwa kazi hii ingefanywa na Roho wa Mungu, basi usingekuwa ushindi dhidi ya Shetani. Roho kiasili huwa ameinuliwa sana kuliko viumbe wenye mwili wa kufa, na Roho wa Mungu ni mtakatifu kwa asili, na anaushinda mwili. Ikiwa Roho angefanya kazi hii moja kwa moja, Asingeweza kuhukumu kutotii kote kwa mwanadamu, na asingeweza kufichua hali nzima ya mwanadamu ya kutokuwa na haki. Kwa maana kazi ya hukumu pia inafanywa kwa mitazamo ya mwanadamu juu ya Mungu, na mwanadamu hajawahi kuwa na dhana yoyote juu ya Roho, na hivyo Roho hana uwezo wa kufunua hali ya mwanadamu ya kutokuwa na haki, wala kuweza kuweka wazi kabisa hali hiyo ya kutokuwa na haki. Mungu mwenye mwili ni adui wa wale wote wasiomjua. Kupitia kuhukumu dhana za mwanadamu na kumpinga, Anafunua hali yote ya kutotii ya mwanadamu. Matokeo ya kazi Yake katika mwili yapo dhahiri zaidi kuliko yale ya kazi ya Roho. Na hivyo, hukumu ya wanadamu wote haifanywi moja kwa moja na Roho, bali ni kazi ya Mungu mwenye mwili. Mungu mwenye mwili anaweza kuonekana na kuguswa na mwanadamu, na Mungu mwenye mwili anaweza kumshinda kabisa mwanadamu. Katika uhusiano wake na Mungu mwenye mwili, mwanadamu huwa anapiga hatua kutoka katika upinzani na kuwa mtii, kutoka katika mateso na kukubaliwa, kutoka katika mitazamo na kuwa na maarifa, na kutoka kukataliwa hadi upendo. Haya ni matokeo ya kazi ya Mungu mwenye mwili. Mwanadamu anaokolewa tu kwa kukubali hukumu Yake, bali hatua kwa hatua tu atamwelewa taratibu kupitia neno la mdomo Wake, ametwaliwa na Yeye wakati wa upinzani wake Kwake, na anapata uzima kutoka Kwake wakati wa kukubali kuadibu Kwake. Hii yote ni kazi ya Mungu mwenye mwili, na sio kazi ya Mungu katika utambulisho Wake kama Roho. Kazi inayofanywa

na Mungu mwenye mwili ni kazi kubwa sana, na ni kazi ya kina sana, na sehemu muhimu ya hatua tatu za kazi ya Mungu ni hatua mbili za kazi ya kupata mwili. Upotovu wa kina wa mwanadamu ni kikwazo kikubwa sana katika kazi ya Mungu mwenye mwili. Hasa, kazi inayofanywa kwa watu wa siku za mwisho ni ngumu sana, na mazingira ni ya uhasama, na ubora wa tabia ya kila aina ya mwanadamu ni duni sana. Lakini mwishoni mwa kazi hii, bado itapokea matokeo mazuri, bila dosari yoyote; haya ni matokeo ya kazi ya mwili, na matokeo haya yanashawishi sana kuliko kazi ile ya Roho. Hatua tatu za kazi ya Mungu zitahitimishwa katika mwili, na lazima zikamilishwe na Mungu mwenye mwili. Kazi muhimu sana imefanywa katika mwili, na wokovu wa mwanadamu ni lazima ufanywe na Mungu mwenye mwili. Ingawa binadamu wote wanahisi kwamba Mungu katika mwili hahusiani na mwanadamu, kwa kweli ni kuwa mwili huu unahusiana na majaliwa na uwepo wa wanadamu wote.

Kila hatua ya kazi ya Mungu ni kwa ajili ya wanadamu wote, na inawalenga wanadamu wote. Ingawa ni kazi Yake katika mwili, bado inaelekezwa kwa binadamu wote; Yeye ni Mungu wa binadamu wote, na ni Mungu wa viumbe vyote vilivyoubwa na ambavyo havijaumbwa. Ingawa kazi Yake katika mwili ipo ndani ya mawanda finyu, na kusudi la kazi hii pia lina mipaka, kila wakati Anapokuwa mwili kufanya kazi Yake, Yeye huchagua chombo cha kazi Yake ambacho ni wakilishi na ambacho kina uwakilishi mkubwa; Hachagui kikundi cha watu wa kawaida na wasiosifika kwa ajili ya kuwafanyiza kazi, lakini badala yake huwachagua kama wawakilishi wa kazi Yake kundi la watu wenye uwezo kuwa wawakilishi wa kazi Yake katika mwili. Kundi hili la watu linachaguliwa kwa sababu ya mawanda ya kazi Yake katika mwili ni finyu, na wamejiandaa mahususi kwa ajili ya Kufanyika Kwake kuwa mwili, na limechaguliwa hasa kwa ajili ya kazi Yake katika mwili. Uchaguzi wa Mungu wa walengwa wa kazi Yake si usio na msingi, bali kulingana na kanuni: Mlengwa wa kazi anapaswa kuwa na manufaa katika kazi ya Mungu mwenye mwili, na anapaswa kuwa na uwezo wa kuwawakilisha wanadamu wote. Kwa mfano, Wayahudi waliweza kuwawakilisha binadamu wote katika kupokea wokovu binafsi wa Yesu, na Wachina wanaweza kuwawakilisha wanadamu wote katika kuukubali ushindi binafsi wa Mungu mwenye mwili. Kuna msingi kwa Wayahudi kuwa wawakilishi wa binadamu wote, na kuna msingi kwa uwakilishi wa Wachina wa wanadamu wote katika kuukubali ushindi binafsi wa Mungu. Hakuna kinachofichua maana ya ukombozi kuliko kazi ya ukombozi iliyofanywa miongoni mwa Wayahudi, na hakuna kinachofichua uhakika na mafanikio ya kazi ya ushindi kuliko kazi ya ushindi iliyofanywa miongoni mwa Wachina. Kazi na neno la Mungu mwenye mwili vinaonekana kuelekezwa kwa kikundi kidogo tu cha watu, lakini kwa hakika, kazi Yake miongoni mwa kikundi hiki kidogo ni kazi ya ulimwengu wote, na neno Lake limeelekezwa kwa wanadamu wote. Baada ya kazi Yake katika mwili kufikia kikomo, wale wanaomfuata wataanza kueneza kazi ambayo Amefanya miongoni mwao. Kitu kizuri zaidi

kuhusu kazi Yake katika mwili ni kwamba anaweza kuacha maneno sahihi na ushawishi, na mapenzi Yake mahususi kwa mwanadamu kwa wale wanaomfuata, ili kwamba hapo baadaye wafuasi Wake waweze kueneza kazi Yake yote katika mwili kwa usahihi zaidi na kwa udhabiti na mapenzi Yake kwa wanadamu wote kwa wanaoikubali njia hii. Ni kazi ya Mungu mwenye mwili pekee miongoni mwa wanadamu ndiyo inayokamilisha ukweli wa Mungu kuwepo na kuishi pamoja na mwanadamu. Ni kazi hii pekee ndiyo inayotimiza shauku ya mwanadamu kuutazama uso wa Mungu, kushuhudia kazi ya Mungu, na kusikia neno la Mungu. Mungu mwenye mwili anahitimisha enzi ambapo Yehova alionekana mgongo tu, na pia anahitimisha enzi ya mwanadamu kuamini katika Mungu asiye dhahiri. Kwa umahususi, kazi ya Mungu mwenye mwili wa mwisho inawaleta wanadamu wote katika enzi ambayo ni halisi zaidi, ya utendaji zaidi na nzuri zaidi. Hahitimishi tu enzi ya sheria na mafundisho ya kidini; la umuhimu zaidi, Anamfunulia mwanadamu Mungu ambaye ni halisi na wa kawaida ambaye ni mwenye haki na mtakatifu, ambaye anafungua kazi ya mpango wa usimamizi na kuonyesha siri za hatma ya mwanadamu, ambaye alimuumba mwanadamu na kuhitimisha kazi ya usimamizi, na ambaye amebakia sirini kwa maelfu ya miaka. Anahitimisha enzi ya Mungu asiye yakini, Anahitimisha enzi ambayo kwayo wanadamu wote wanatamani kuutafuta uso wa Mungu lakini wanashindwa, Anahitimisha enzi ambayo kwayo wanadamu wote wanamtumikia Shetani, na Anawaongoza wanadamu wote katika enzi mpya kabisa. Haya yote ni matokeo ya Mungu mwenye mwili kwa niaba ya Roho wa Mungu. Wakati Mungu anapofanya kazi katika mwili Wake, wale wanaomfuata wanakuwa hawatafuti tena vitu hivyo ambavyo vinaonekana kuishi na kutoishio, na wao wanaacha kukisia mapenzi ya Mungu asiye yakini. Mungu anapoeneza kazi Yake katika mwili, wale wanaomfuata wataieneza kazi ambayo Ameifanya katika mwili kwa dini na madhehebu yote, na watazungumza maneno Yake yote katika masikio ya wanadamu wote. Yote yale yanayosikizwa na wale wanaoipokea injili Yake yatakuwa ni ukweli wa kazi Yake, yatakuwa mambo ambayo mwanadamu ameyashuhudia na kuyaona binafsi, na utakuwa ukweli na sio uvumi. Ukweli huu ni ushahidi ambao Anauenzeza kazi na pia ni zana ambazo Anazitumia katika kueneza kazi. Bila uwepo wa ukweli, injili Yake isingeweza kuenea katika nchi zote na maeneo yote; bila ukweli bali kwa fikira tu za mwanadamu, Asingeweza kufanya kazi ya kuushinda ulimwengu wote. Roho hagusiki na mwanadamu, na wala haonekani kuonekana na mwanadamu, na kazi ya Roho haiwezi kuacha ushahidi au ukweli wowote zaidi wa kazi ya Mungu kwa ajili ya mwanadamu. Mwanadamu kamwe hataweza kuuona uso halisi wa Mungu, na siku zote ataamini katika Mungu asiye yakini ambaye hayupo. Mwanadamu hataweza kuutazama uso wa Mungu, hataweza kusikia maneno yaliyozungumzwa na Mungu moja kwa moja. Mawazo ya mwanadamu, hata hivyo, ni matupu, na hayawezi kuchukua nafasi ya uso halisi wa Mungu; tabia ya asili ya Mungu, na kazi ya Mungu Mwenyewe haiwezi kuigwa na mwanadamu. Mungu wa mbinguni asiyeonekana na kazi Yake inaweza kuletwa tu duniani na

Mungu mwenye mwili ambaye binafsi Anafanya kazi Yake miongoni mwa wanadamu. Hii ndiyo njia halisi ambayo Mungu anaonekana kwa mwanadamu, ambayo kwayo mwanadamu anamwona Mungu na kuujua uso wa kweli wa Mungu, na haiwezi kufanikishwa na Mungu asiye kuwa katika mwili. Baada ya Mungu kufanya kazi Yake hadi hatua hii, kazi Yake tayari imeshafanikiwa kuwa na matokeo mazuri, na imekuwa ni mafanikio kamili. Kazi binafsi ya Mungu mwenye mwili tayari imekwishakamilisha asilimia tisini ya kazi ya usimamizi Wake mzima. Mwili umetoa mwanzo mzuri katika kazi Yake yote, na muhtasari kwa ajili ya kazi Yake yote, na umetangaza kazi Yake yote na Ameifanya ya mwisho kupitia ujazaji tena wa kazi hii yote. Kuanzia sasa, hakutakuwepo na Mungu mwingine katika mwili kwa ajili ya kufanya hatua ya nne ya kazi ya Mungu, na hakutakuwa na kazi ya miujiza zaidi ya kupata mwili kwa tatu kwa Mungu.

Kila hatua ya kazi ya Mungu katika mwili inawakilisha kazi Yake ya enzi yote, na haiwakilishi kipindi fulani kama kazi ya mwanadamu. Na hivyo mwisho wa kazi ya kufanyika Kwake mwili mara ya mwisho haimaanishi kwamba kazi Yake imefikia mwisho kabisa, kwa maana kazi Yake katika mwili inawakilisha enzi yote, na haiwakilishi kipindi tu ambacho Anafanya kazi Yake katika mwili tu. Ni kwamba tu Anakamilisha kazi Yake ya enzi yote wakati ambapo yupo katika mwili, ambayo baadaye inaenea sehemu zote. Baada ya Mungu mwenye mwili kutimiza huduma yake, atawakabidhi wale wote wanaoifuata kazi Yake ya baadaye. Kwa njia hii kazi Yake ya enzi yote itaendelezwa bila kusitishwa. Kazi ya enzi yote ya kufanyika kuwa mwili itachukuliwa tu kuwa imekamilika baada ya kuenea ulimwenguni kote. Kazi ya Mungu mwenye mwili huanzisha enzi mpya, na wale wanaoiendeleza kazi Yake ni watu wanaotumiwa naye. Kazi inayofanywa na mwanadamu yote ipo ndani ya huduma ya Mungu mwenye mwili, na haina uwezo wa kwenda zaidi ya mawanda haya. Ikiwa Mungu mwenye mwili haji kufanya kazi Yake, mwanadamu hana uwezo wa kuhitimisha enzi ya zamani, na hana uwezo wa kuikaribisha enzi mpya. Kazi inayofanywa na mwanadamu ipo tu ndani ya wajibu wake ambao unawezekana kibinadamu, na haiwakilishi kazi ya Mungu. Ni Mungu mwenye mwili pekee ndiye anayeweza kuja na kukamilisha kazi ambayo Anapaswa kuifanya, na mbali na Yeye, hakuna anayeweza kuifanya kazi hii badala Yake. Bila shaka, kile Ninachozungumzia ni kuhusiana na kazi ya kufanyika mwili. Huyu Mungu mwenye mwili, kwanza anachukua hatua ya kazi ambayo haipatani na mitazamo ya mwanadamu, baada ya hapo Anafanya kazi zaidi ambayo haipatani na mitazamo ya mwanadamu. Lengo la kazi hii ni kumshinda mwanadamu. Kwa upande mmoja, kupata mwili kwa Mungu hakupatani na dhana za mwanadamu, aidha, Anafanya kazi zaidi ambayo haipatani na dhana za mwanadamu, na kwa hivyo mwanadamu anakuza mawazo zaidi ya kukosoa kumhusu. Anafanya kazi ya ushindi miongoni mwa wanadamu ambaye ana dhana nyingi sana kumhusu. Bila kujali jinsi wanavyomchukulia, Atakapokuwa

amekamilisha huduma Yake, wanadamu wote watakuwa chini ya utawala Wake. Ukweli wa kazi hii hauonekani tu miongoni mwa Wachina, bali wao wanawakilisha namna ambavyo wanadamu wote watakavyoshindwa. Matokeo yanayoonekana kwa watu hawa ni kitangulizi cha matokeo yatakayoonekana kwa wanadamu wote, na matokeo ya kazi Anayofanya wakati ujao yatazidi sana matokeo kwa watu hawa. Kazi ya Mungu katika mwili haihusishi mshindo mkubwa wa tarumbeta, wala imefunikwa katika maficho. Ni halisi na ya kweli, na ni kazi ambayo moja kujumlisha na moja ni sawa sawa na mbili. Hajafichwa kwa mtu yeyote, na wala haimdanganyi mtu yeyote. Kile ambacho watu wanaona ni vitu halisi, na kile ambacho mwanadamu anapata ni ukweli halisi na maarifa. Kazi itakapokamilika, mwanadamu atakuwa na maarifa mapya juu Yake, na wale ambao kweli wanamtafuta Mungu hawatakuwa na dhana zozote juu Yake. Haya siyo tu matokeo ya kazi Yake kwa Wachina, lakini pia inawakilisha matokeo ya kazi Yake katika kuwashinda wanadamu wote, kwa maana hakuna kitu ambacho ni cha manufaa zaidi katika kazi ya kuwashinda watu kuliko mwili huu, na kazi ya mwili huu, na kila kitu cha mwili huu. Vina manufaa katika kazi Yake leo, na vina manufaa katika kazi Yake hapo baadaye. Mwili huu utawashinda wanadamu wote na utawapata wanadamu wote. Hakuna kazi bora zaidi ambayo kwayo wanadamu wote watamwona Mungu, na kumtii Mungu, na kumfahamu Mungu. Kazi inayofanywa na mwanadamu inawakilisha tu mawanda finyu, na Mungu anapofanya kazi Yake hazungumzi na watu fulani, bali Anazungumza na wanadamu wote, na wale wote wanaoikubali kazi Yake. Mwisho Anaoutangaza ni mwisho wa wanadamu wote, na sio mwisho wa mtu fulani tu. Hamtendei mtu yeyote kwa umahususi, wala hampendelei mtu yeyote, na Anafanya kazi kwa ajili ya, na Anazungumza na wanadamu wote. Na kwa hiyo Mungu huyu katika mwili amekwisha waainisha wanadamu wote kulingana na aina yao, tayari amekwisha wauhukumu wanadamu wote, na amekwishapangilia hatima inayofaa kwa wanadamu wote. Ingawa Mungu anafanya kazi Yake China tu, kwa hakika Ameshaamua kazi ya ulimwengu mzima. Hawezi kusubiri hadi kazi Yake itakapoenea miongoni mwa wanadamu wote kabla ya kutoa matamko Yake na kuweka mipango hatua kwa hatua. Hivyo, sio kwamba utakuwa umechelewa sana? Sasa Anaweza kabisa kukamilisha kazi ya wakati ujao kabla ya wakati huo. Kwa sababu Yule anayefanya kazi ni Mungu mwenye mwili, Anafanya kazi isiyokuwa na mipaka ndani ya mawanda yenye mipaka, na baadaye Atamfanya mwanadamu atekeleze jukumu ambalo mwanadamu anapaswa kulitekeleza; hii ni kanuni ya kazi Yake. Anaweza kuishi tu na mwanadamu kwa muda, na hawezi kuambatana na mwanadamu hadi kazi ya enzi zote itakapokamilika. Ni kwa sababu Yeye ni Mungu kwamba Yeye hutabiri kazi Yake ya Wakati ujao kabla ya wakati. Baada ya hapo, Atawaainisha wanadamu wote kulingana na aina kwa maneno Yake, na mwanadamu ataingia katika kazi Yake ya hatua kwa hatua kulingana na neno Lake. Hakuna atakayekwepa, na wote wanapaswa kutenda kulingana na hili. Hivyo, katika wakati ujao, enzi itaongozwa na maneno Yake, na sio kuongozwa na Roho.

Kazi ya Mungu katika mwili ni lazima ifanywe katika mwili. Kama ingefanywa moja kwa moja na Roho wa Mungu isingeweza kutoa matokeo yoyote. Hata kama ingefanywa na Roho, kazi hii isingekuwa na maana kubwa, na hatimaye isingekuwa na ushawishi. Viumbe vyote vinatamani kujua iwapo kazi ya Muumbaji ina maana, na inawakilisha kitu gani, na ni kwa ajili ya nini, na iwapo kazi ya Mungu ina mamlaka kamili na hekima, na endapo ina thamani na maana ya kina. Kazi Anayofanya ni kwa ajili ya wokovu wa wanadamu wote, kwa ajili ya kumshinda Shetani, na kwa kuwa na ushuhuda wa Mungu miongoni mwa vitu vyote. Hivyo, kazi Anayofanya ni lazima iwe ya umuhimu mkubwa. Mwili wa mwanadamu umepotoshwa na Shetani, na wengi wamepofushwa, na kuumizwa sana. Sababu muhimu sana ambayo inamfanya Mungu kufanya kazi katika mwili ni kwa sababu mlengwa wa wokovu Wake ni mwanadamu, ambaye ni wa mwili, na kwa sababu Shetani pia anatumia mwili wa mwanadamu kusumbua kazi ya Mungu. Vita na Shetani kwa hakika ni kazi ya kumshinda mwanadamu, na wakati uo huo mwanadamu pia ni mlengwa wa wokovu wa Mungu. Kwa njia hii, kazi ya Mungu mwenye mwili ni muhimu. Shetani aliupotosha mwili wa mwanadamu, na mwanadamu akawa mfano halisi wa Shetani, na akawa mlengwa wa kushindwa na Mungu. Kwa njia hii, kazi ya kupambana na Shetani na kumwokoa mwanadamu inatokea duniani, na Mungu ni lazima awe mwanadamu ili aweze kupambana na mwanadamu. Hii ni kazi yenye utendaji wa hali ya juu. Mungu anapofanya kazi katika mwili, kwa hakika Anapambana na Shetani katika mwili. Anapofanya kazi katika mwili, Anafanya kazi Yake katika ulimwengu wa kiroho, na Anafanya kazi Yake yote katika ufalme wa kiroho ili iwe halisi duniani. Anayeshindaniwa ni mwanadamu, asiye mtiifu Kwake, yule anayeshindwa ni mfano halisi wa Shetani (bila shaka, huyu pia ni mwanadamu), ambaye ana uadui na Yeye, na ambaye ataokolewa hatimaye ni mwanadamu. Kwa namna hii, ni muhimu zaidi Kwake kuwa mwanadamu ambaye ana ganda la nje la kiumbe, ili kwamba Awe na uwezo wa kupambana na Shetani katika uhalisi, kumshinda mwanadamu, ambaye si mtiifu Kwake na ambaye ana kuonekana kwa nje ambako kunafanana na Yeye, na kumwokoa mwanadamu, ambaye ana umbo la nje kama Lake na aliyeumizwa na Shetani. Adui Wake ni mwanadamu, mlengwa wa ushindi Wake ni mwanadamu, na mlengwa wa wokovu Wake ni mwanadamu, aliyeumbwa na Yeye. Hivyo ni lazima Awe mwanadamu, na kwa njia hii, kazi Yake inakuwa rahisi zaidi. Ana uwezo wa kumshinda Shetani na kumshinda mwanadamu, aidha, anaweza kumwokoa mwanadamu. Ingawa mwili huu ni wa kawaida na halisi, Yeye si mwili wa kawaida. Yeye si mwili ambao ni mwanadamu tu, bali mwili ambao una uanadamu na uungu. Hii ndiyo tofauti Yake na mwanadamu, na ni alama ya utambulisho wa Mungu. Ni mwili tu kama huu ndio unaweza kufanya kazi Anayokusudia kufanya, na kutimiza huduma ya Mungu katika mwili, na kukamilisha kazi Yake miongoni mwa wanadamu. Isingekuwa hivyo, kazi Yake miongoni mwa wanadamu ingekuwa tupu na yenye dosari. Ingawa Mungu anaweza kupambana na roho wa Shetani na kuibuka mshindi, asili ya zamani ya mwanadamu aliyepotoka haiwezi

kuondolewa, na wale ambao sio watiifu Kwake na wanaompinga hawawezi kuwa wahusika katika utawala Wake, ambayo kusema, Hawezi kamwe kumshinda mwanadamu, na hawezi kamwe kuwapata wanadamu wote. Kama kazi Yake duniani haiwezi kutatuliwa, basi usimamizi Wake hautafika mwisho, na wanadamu wote hawataweza kuingia katika pumziko. Kama Mungu hawezi kuingia katika pumziko pamoja na viumbe Wake wote, basi hakutakuwa na matokeo ya usimamizi huo, na utukufu wa Mungu kwa sababu hiyo utatoweka. Ingawa mwili Wake hauna mamlaka, kazi Anayofanya itapokea matokeo yake. Huu ndio mwelekeo usioepukika wa kazi Yake. Haijalishi kama mwili Wake una mamlaka au la, maadamu Ana uwezo wa kufanya kazi ya Mungu Mwenyewe, basi Yeye ni Mungu Mwenyewe. Haijalishi mwili huu ni wa kawaida kiasi gani, Anaweza kufanya kazi Anayopaswa kufanya, maana mwili huu ni Mungu na wala si mwanadamu tu. Sababu ambayo mwili huu unaweza kufanya kazi ambayo mwanadamu hawezi kufanya ni kwamba kiini Chake cha ndani si kama cha mwanadamu yeyote yule, na sababu kuwa Anaweza kumwokoza mwanadamu ni kuwa utambulisho Wake ni tofauti na wa mwanadamu yeyote yule. Mwili huu ni muhimu sana kwa mwanadamu kwa sababu ni mwanadamu hata zaidi ni Mungu, kwa sababu Anaweza kufanya kazi ambayo hakuna mwanadamu wa kawaida anayeweza kufanya, na kwa sababu Anaweza kumwokoza mwanadamu aliyepotoka, ambaye anaishi pamoja na Yeye duniani. Ingawa Anafanana na mwanadamu, Mungu mwenye mwili ni wa muhimu sana kwa mwanadamu kuliko mtu yeyote wa thamani, kwa maana Anaweza kufanya kazi ambayo haiwezi kufanywa na Roho wa Mungu, ni mwenye uwezo zaidi kuliko Roho wa Mungu kuwa na ushuhuda kwa Mungu Mwenyewe, na ni mwenye uwezo zaidi kuliko Roho wa Mungu kuweza kumpata mwanadamu kabisa. Kwa sababu hii, ingawa mwili huu ni wa kawaida, mchango Wake kwa wanadamu na umuhimu Wake katika uwepo wa mwanadamu kunamfanya Awe wa thamani zaidi, na thamani halisi na umuhimu wa mwili huu hauwezi kupimwa na mwanadamu yeyote. Ingawa mwili huu hauwezi kumwangamiza Shetani moja kwa moja, Anaweza kutumia kazi Yake kumshinda mwanadamu na kumshinda Shetani, na kumfanya Shetani kutii kikamilifu katika utawala Wake. Ni kwa sababu Mungu amepata mwili ili kwamba Aweze kumshinda Shetani na aweze kumwokoza binadamu. Hamwangamizi Shetani moja kwa moja, bali Anakuwa mwili ili kuweza kufanya kazi ya kumshinda binadamu, ambaye amepotoshwa na Shetani. Kwa njia hii, Anakuwa na uwezo zaidi wa kuwa ushuhuda Kwake Mwenyewe miongoni mwa viumbe, na Anakuwa na uwezo zaidi wa kumwokoza mwanadamu aliyepotea. Ushindi wa Mungu mwenye mwili dhidi ya Shetani unabeba ushuhuda mkubwa, na una ushawishi mkubwa, kuliko uangamizaji wa Shetani wa moja kwa moja na Roho wa Mungu. Mungu katika mwili Ana uwezo zaidi wa kumsaidia mwanadamu kumjua Muumba, na Ana uwezo zaidi wa kuwa na ushuhuda Wake mwenyewe miongoni mwa viumbe.

Kiini cha Mwili Ulio na Mungu

Mungu katika kupata mwili Kwake mara ya kwanza Aliishi duniani kwa miaka thelathini na tatu na nusu, lakini Alitekeleza huduma Yake kwa miaka mitatu na nusu pekee ya hiyo miaka yote. Kipindi Alichofanya kazi na kabla Aanze kazi Yake, Alikuwa na ubinadamu wa kawaida. Aliishi na ubinadamu Wake wa kawaida kwa miaka thelathini na tatu na nusu. Katika miaka yote mitatu na nusu ya mwisho Alijifichua kuwa Mungu mwenye mwili. Kabla Aanze kutekeleza kazi ya huduma Yake, Alikuwa na ubinadamu wa kawaida, bila kuonyesha ishara ya uungu Wake, na ni baada tu ya kuanza rasmi kutekeleza huduma Yake ndipo uungu Wake uliwekwa wazi. Maisha na kazi Zake katika ile miaka ishirini na tisa yote ilidhihirisha kuwa Alikuwa mwanadamu halisi, mwana wa Adamu, mwili; kwani huduma Yake ilianza tu kwa dhati baada ya umri wa miaka ishirini na tisa. Maana ya kupata mwili ni kwamba Mungu Anajionyesha katika mwili, na Anakuja kufanya kazi miongoni mwa wanadamu wa uumbaji Wake katika umbo la mwili. Hivyo, ili Mungu kuwa mwili, ni lazima kwanza Apate umbo la mwili, mwili wenye ubinadamu wa kawaida; hili ndilo hitaji la kimsingi zaidi. Kwa kweli, maana ya kupata mwili kwa Mungu ni kwamba Mungu Anaishi na kufanya kazi katika mwili, Mungu katika kiini Chake Anakuwa mwili, Anakuwa mwanadamu. Maisha Yake ya kimwili na kazi vinaweza kugawanywa katika hatua mbili. Kwanza ni maisha Anayoishi kabla ya kuanza kutekeleza huduma Yake. Anaishi katika familia ya kawaida ya binadamu, katika ubinadamu wa kawaida kabisa, Akifuata maadili na sheria za maisha ya wanadamu, Akiwa na mahitaji ya kawaida ya binadamu (chakula, nguo, makazi, na usingizi), na udhaifu wa kawaida wa binadamu na hisia za kawaida za binadamu. Kwa maneno mengine, katika hatua hii ya kwanza Anaishi maisha yasiyo na uungu, ubinadamu wa kawaida kabisa, Akijishughulisha na shughuli zote za wanadamu. Hatua ya pili ni ya maisha Anayoishi baada ya kuanza kutekeleza huduma Yake. Bado Yumo katika ubinadamu wa kawaida Akiwa na umbo la nje la binadamu bila kuonyesha ishara isiyo ya kawaida kwa nje. Lakini kimsingi Anaishi kwa ajili ya huduma Yake, na wakati huu ubinadamu Wake wa kawaida upo kikamilifu kuhudumia kazi ya kawaida ya uungu Wake; kwani wakati huo, ubinadamu Wake wa kawaida umekomaa kiasi cha kuweza kutekeleza huduma Yake. Kwa hivyo hatua ya pili ya maisha Yake ni ya kutekeleza huduma Yake katika ubinadamu Wake wa kawaida, ni maisha ya ubinadamu wa kawaida na uungu kamili. Sababu ya kuishi katika maisha ya kawaida kabisa ya ubinadamu katika hatua ya kwanza ya maisha Yake ni kwamba ubinadamu Wake bado ulikuwa haujalilingana na ukamilifu wa kazi ya uungu, bado haujakomaa; ni baada tu ya kukomaa kwa ubinadamu Wake na kuwa na uwezo wa kustahimili huduma Yake, ndipo Anaweza kuanza kutekeleza huduma Yake. Kwa kuwa Yeye, kama mwili, Anahitaji kukua na kukomaa, hatua ya kwanza ya maisha Yake ni ile ya ubinadamu wa kawaida, ilhali katika hatua ya pili, kwa kuwa ubinadamu Wake una uwezo wa kuanza kazi Yake na kutekeleza huduma Yake, maisha ambayo Mungu mwenye mwili Anaishi katika kipindi cha huduma Yake ni ya ubinadamu na ya uungu kamili. Iwapo Mungu mwenye mwili Angeanza huduma Yake kwa dhati

tangu kuzaliwa kwake, na kufanya ishara na maajabu ya mwujiza, basi Asingekuwa na kiini cha kimwili. Kwa hivyo, ubinadamu Wake upo kwa sababu ya kiini chake cha Kimwili; hakuwezi kuwepo na mwili bila ubinadamu, na mtu bila ubinadamu si mwanadamu. Kwa njia hii, ubinadamu wa mwili wa Mungu ni sifa ya ndani ya mwili wa Mungu. Kusema kwamba “Mungu Anapokuwa mwili Anakuwa na uungu kamili, na si binadamu kabisa,” ni kufuru, kwa kuwa kauli hii haipo kabisa, na hukiuka kanuni ya Yesu kupata mwili. Hata baada ya kuanza kutekeleza huduma Yake, bado Anaishi katika uungu Wake akiwa na umbo la nje la binadamu Anapofanya kazi Yake; ni kwamba tu wakati huo, ubinadamu Wake una kusudi la pekee la kuuwezesha uungu Wake kutekeleza kazi katika mwili wa kawaida. Kwa hivyo wakala wa kazi ni uungu unaosetiriwa katika ubinadamu Wake. Ni uungu na wala si ubinadamu Wake unaofanya kazi, lakini ni uungu uliojificha katika ubinadamu Wake; kimsingi kazi Yake inafanywa na uungu Wake kikamilifu, haifanywi na ubinadamu Wake. Ila mtekelezaji wa kazi ni mwili Wake. Mtu anaweza kusema kuwa Yeye ni mwanadamu na vilevile Mungu, kwani Mungu Anakuwa Mungu Anayeishi katika mwili, mwenye umbo la mwanadamu na kiini cha binadamu lakini pia na kiini cha Mungu. Kwa sababu ni mwanadamu mwenye kiini cha Mungu, Yuko juu ya wanadamu wote walioumbwa, juu ya mwanadamu yeyote anayeweza kutekeleza kazi ya Mungu. Kwa hivyo, miongoni mwa wale wote walio na umbo la binadamu kama Lake, miongoni mwa wale wote walio na ubinadamu, Yeye pekee ndiye Mungu mwenye mwili Mwenyewe—wengine wote ni wanadamu walioumbwa. Japokuwa wote wana ubinadamu, wanadamu walioumbwa hawana chochote ila ubinadamu, ilhali Mungu mwenye mwili ni tofauti: katika mwili Wake, si tu kwamba ana ubinadamu ila pia muhimu zaidi Ana uungu. Ubinadamu Wake waweza kuonekana katika mwonekano wa nje wa Mwili Wake na katika maisha Yake ya kila siku; ila uungu Wake ni vigumu kuonekana. Kwa kuwa uungu Wake huonyeshwa pale tu Anapokuwa na ubinadamu, na si wa kimuujiza kama watu wanavyoukisia kuwa, ni vigumu sana kwa watu kuuona. Hata leo hii ni vigumu sana kwa watu kuelewa kiini cha kweli cha Mungu mwenye mwili. Kwa kweli, hata baada ya Mimi kulizungumzia kwa mapana, Natarajia bado liwe fumbo kwa wengi wenu. Suala hili ni rahisi sana: kwa kuwa Mungu Anakuwa mwili, kiini Chake ni muungano wa ubinadamu na uungu. Muungano huu unaitwa Mungu Mwenyewe, Mungu Mwenyewe duniani.

Maisha Aliyoishi Yesu duniani yalikuwa maisha ya kimwili ya kawaida. Aliishi katika ubinadamu wa kawaida wa mwili Wake. Mamlaka Yake—kufanya kazi Yake na kuzungumza neno Lake, au kuwaponya wagonjwa au kufukuza mapepo, kufanya hiyo kazi isiyo ya kawaida—hayakujitokeza, kwa kiasi kikubwa, hadi Alipoanza huduma Yake. Maisha Yake kabla ya umri wa miaka ishirini na tisa, kabla ya Yeye kuanza kutekeleza huduma Yake, yalikuwa uthibitisho tosha kuwa Alikuwa mwili wa kawaida. Kwa sababu ya hili, na kwa kuwa

Alikuwa bado Hajaanza kutekeleza huduma Yake, watu hawakuona chochote cha uungu ndani Yake, hawakuona chochote zaidi ya ubinadamu wa kawaida, mwanadamu wa kawaida—kama vile wakati ule baadhi ya watu walimwamini kuwa mwana wa Yosefu. Watu walidhani kuwa Alikuwa mwana wa mwanadamu wa kawaida, hawakuwa na njia ya kugundua kuwa Alikuwa mwili wa Mungu; hata wakati Alipotenda miujiza mingi katika harakati za kutekeleza huduma Yake, watu wengi bado walisema Alikuwa mwana wa Yosefu, kwani Alikuwa Kristo mwenye umbo la nje la ubinadamu wa kawaida. Ubinadamu Wake wa kawaida pamoja na kazi yake vyote vilikuwepo ili kutimiza umuhimu wa kupata mwili kwa mara ya kwanza, kuthibitisha kuwa Mungu Alikuwa Amekuja katika mwili kwa ukamilifu, kuwa mwanadamu wa kawaida kabisa. Kuwa na ubinadamu wa kawaida kabla ya kuanza kazi Yake ulikuwa uthibitisho kuwa Alikuwa mwili wa kawaida; na kwa kuwa Alifanya kazi baadaye lilithibitisha pia kuwa Alikuwa mwili wa kawaida, kwa kuwa Alifanya ishara na miujiza, kuponya wagonjwa na kufukuza mapepo katika mwili na ubinadamu wa kawaida. Sababu za kufanya miujiza ilikuwa kwamba mwili Wake ulikuwa umebeba mamlaka ya Mungu, ulikuwa mwili ambamo Roho wa Mungu Alikuwa Amesetiriwa. Alikuwa na mamlaka haya kwa sababu ya Roho wa Mungu, na haikumaanishi kuwa Hakuwa Mwili. Kuponya wagonjwa na kufukuza mapepo ilikuwa kazi Aliyopaswa kutekeleza katika huduma Yake, onyesho la uungu Wake uliojificha ndani ya ubinadamu Wake, na haijalishi ni ishara za aina gani Alionyesha au Alidhihirisha vipi mamlaka Yake, bado Aliishi katika ubinadamu wa kawaida na bado Alikuwa mwili wa kawaida. Aliishi katika mwili wa kawaida mpaka wakati Alipofufuliwa baada ya kufa msalabani. Aliishi katika mwili wa kawaida. Akitoa neema, Akiwaponya wagonjwa, na kufukuza mapepo hayo yote yalikuwa sehemu ya huduma Yake, hiyo yote ilikuwa kazi Aliyotekeleza katika mwili Wake wa kawaida. Kabla ya kwenda msalabani, Hakuuacha mwili Wake wa kawaida, haijalishi Alikuwa Anafanya nini. Alikuwa Mungu Mwenyewe, Akifanya kazi ya Mungu, lakini kwa sababu Alikuwa Mwili wa Mungu, Alikula chakula na kuvaa nguo, Alikuwa na mahitaji ya kawaida ya binadamu, Alikuwa na fikira za kawaida za binadamu na akili za kawaida. Haya yote yalikuwa uthibitisho kwamba Alikuwa mwanadamu wa kawaida, ambayo yalithibitisha kuwa mwili wa Mungu ulikuwa mwili wenye ubinadamu wa kawaida, haukuwa wa rohani. Kazi Yake ilikuwa kukamilisha kazi ya Mungu kupata mwili mara ya kwanza, kutimiza huduma ya kupata mwili mara ya kwanza. Umuhimu wa kupata mwili ni kwamba mtu wa kawaida Anatekeleza kazi ya Mungu Mwenyewe; yaani, kwamba Mungu Anatekeleza kazi Yake ya uungu katika ubinadamu na hivyo kumshinda Shetani. Kupata mwili kunamaanisha kwamba Roho wa Mungu Anakuwa Mwili, yaani, Mungu Anakuwa mwili; kazi Anayoifanya katika mwili ni kazi ya Roho, inayothibitika katika mwili, na kuonyeshwa kwa mwili. Hakuna mwingine ila tu mwili wa Mungu Anayeweza kutimiza huduma ya Mungu mwenye mwili; yaani, mwili wa Mungu kuwa mwili pekee, ubinadamu huu wa kawaida—na hakuna mwingine yeyote—anayeweza kuonyesha

kazi ya uungu. Ikiwa, wakati wa kuja Kwake wa kwanza, Mungu Asingekuwa Amekuwa na ubinadamu wa kawaida kabla ya umri wa miaka ishirini na tisa—ikiwa mara tu Alipozaliwa Angeweza kufanya miujiza, ikiwa mara tu Alipojifunza kuongea Angeweza kuongea lugha ya mbinguni, ikiwa mara tu Alipokanyaga duniani Angeweza kuyaelewa mambo yote ya kidunia, kung'amua fikira za kila mtu na nia zao—mtu kama huyu asingeitwa mwanadamu wa kawaida, na mwili Wake usingeitwa mwili wa mwanadamu. Iwapo ingekuwa hivi kwa Kristo, basi maana na kiini cha kuwa mwili kwa Mungu ingepotea. Kuwa Yeye ana ubinadamu wa kawaida kunathibitisha kuwa Yeye ni Mungu Aliyejidhihirisha katika mwili; ukweli kwamba Anapitia ukuaji wa kawaida wa binadamu unaonyesha zaidi kuwa Yeye ni mwili wa kawaida; zaidi, kazi Yake ni uthibitisho tosha kuwa Yeye ni Neno la Mungu, Roho wa Mungu, kuwa mwili. Mungu Anakuwa mwili kwa sababu ya mahitaji ya kazi; kwa maneno mengine, hii hatua ya kazi inapaswa kufanywa kwa mwili, kufanywa katika ubinadamu wa kawaida. Hili ndilo sharti la “Neno kuwa mwili,” la “Neno kuonekana katika mwili,” na ndio ukweli wa Mungu kupata mwili mara Mbili. Watu huenda wakaamini kuwa maisha yote ya Yesu yaliambatana na miujiza, kwamba hadi mwisho wa kazi Yake duniani Hakudhihirisha ubinadamu wa kawaida, kwamba Hakuwa na mahitaji ya kawaida ya mwanadamu au udhaifu au hisia za binadamu, kwamba Hakuhitaji vitu vya kimsingi vya maisha au kuwa na fikira za kawaida za binadamu. Wanadhani tu kuwa Alikuwa mwanadamu asiyekuwa na akili ya kawaida, aliyevuka mipaka ya ubinadamu. Wanaamini kuwa kwa sababu Yeye ni Mungu, Hapaswi kufikiri na kuishi jinsi wanadamu wa kawaida hufanya, kwamba ni mtu wa kawaida tu, mwanadamu halisi, anayeweza kufikiri fikira za mwanadamu wa kawaida na kuishi maisha ya mwanadamu wa kawaida. Haya yote ni mawazo ya wanadamu na maoni ya wanadamu, ambayo yanakinzana na madhumuni asilia ya kazi ya Mungu. Kufikiri kwa mwanadamu wa kawaida kunadumisha mawazo ya kawaida ya mwanadamu na ubinadamu wa kawaida; ubinadamu wa kawaida unadumisha kazi za kawaida za mwili; na kazi za kawaida za mwili zinawezesha maisha ya kawaida ya mwili katika ukamilifu wake. Ni kwa kufanya kazi tu katika mwili kama huo ndipo Mungu Anaweza kutimiza kusudi la kupata mwili Kwake. Kama Mungu mwenye mwili angekuwa na umbo la nje tu la mwili, bila kufikiri fikira za kawaida za binadamu, basi mwili huu usingekuwa na mawazo ya binadamu, sembuse ubinadamu halisi. Ni vipi ambavyo mwili kama huu, usio na ubinadamu, ungeweza kutimiza huduma ambayo Mungu mwenye mwili Anapaswa kutekeleza? Akili za kawaida huwezesha vipengele vyote vya maisha ya binadamu; bila akili ya kawaida, mtu hawezi kuwa mwanadamu. Kwa maneno mengine, mtu asiyefikiria fikira za kawaida ni mgonjwa wa akili. Na Kristo ambaye Hana ubinadamu ila uungu pekee Hawezi kuitwa mwili wa Mungu. Basi, mwili wa Mungu unawezaje kukosa ubinadamu wa kawaida? Je, si kufuru kusema kwamba Kristo hana ubinadamu? Kila shughuli ambazo wanadamu wa kawaida hufanya hutegemea utendaji kazi wa akili ya kawaida ya mwanadamu. Bila hiyo, wanadamu wangukuwa na mienendo iliyopotoka;

wangeshindwa hata kutofautisha kati ya nyeupe na nyeusi, wema na uovu; na hawangekuwa na maadili ya binadamu na kanuni za uadilifu. Vivyo hivyo, iwapo Mungu mwenye mwili Asingefikiri kama mwanadamu wa kawaida, basi Asingekuwa mwili halisi, mwili wa kawaida. Mwili usiofikiri kama huo haungeweza kuikabili kazi ya uungu. Haungeweza kushiriki kwa kawaida katika shughuli za za mwili wa kawaida, sembuse kuishi na wanadamu duniani. Hivyo basi, umuhimu wa Mungu kupata mwili, kiini kabisa cha Mungu kuja duniani, kingepotea. Ubinadamu wa Mungu kuwa mwili huwepo kudumisha kazi ya kawaida ya uungu katika mwili; fikira Zake za kawaida za binadamu zinadumisha ubinadamu Wake wa kawaida na shughuli Zake zote za kimwili. Mtu anaweza kusema kuwa fikira zake za kawaida za binadamu zipo ili kudumisha kazi yote ya Mungu katika mwili. Kama mwili huu usingekuwa na akili ya mwanadamu wa kawaida, basi Mungu Asingefanya kazi katika mwili, na Anachopaswa kufanya kimwili kisingetimilika. Japo Mungu mwenye mwili Ana akili ya mwanadamu wa kawaida, kazi Yake haijatiwa doa na mawazo ya binadamu; Anafanya kazi katika ubinadamu na akili ya kawaida chini ya masharti ya awali kuwa atakuwa na ubinadamu na akili ya kawaida, na si na mawazo ya kawaida ya binadamu. Haijalishi mawazo ya mwili Wake ni bora kiasi gani, kazi Yake haionyeshi alama ya mantiki au kufikiria. Kwa maneno mengine, kazi Yake haiwazwi na akili ya mwili Wake, ila ni onyesho la moja kwa moja la kazi ya uungu katika ubinadamu Wake. Kazi Yake yote ni huduma Anayostahili kutimiza, na haiwazwi hata chembe kwa akili Zake. Kwa mfano, kuponya wagonjwa, kufukuza mapepo na kusulubishwa hayakuwa mazao ya akili Zake za binadamu, yasingeweza kutimizwa na mwanadamu yeyote mwenye akili za binadamu. Vivyo hivyo, kazi ya ushindi ya leo ni huduma ambayo ni sharti itekelezwe na Mungu mwenye mwili, lakini si kazi ya mapenzi ya mwanadamu, ni kazi ambayo uungu Wake unapaswa kufanya, kazi ambayo hakuna mwanadamu wa mwili anaiweza. Kwa hivyo, Mungu mwenye mwili ni lazima Awe na akili za binadamu, ni lazima Awe na ubinadamu wa kawaida, kwa sababu ni lazima Atekeleze kazi Yake katika ubinadamu akiwa na akili za kawaida. Hiki ndicho kiini cha kazi ya Mungu mwenye Mwili, kiini chenyewe cha Mungu mwenye mwili.

Kabla Yesu Hajatekeleza kazi yake, Aliishi tu katika ubinadamu Wake wa kawaida. Hakuna mtu ambaye angeweza kutambua kuwa Alikuwa Mungu, hakuna aliyegundua kuwa Alikuwa Mungu mwenye mwili; watu walimjua tu kama mwanadamu wa kawaida kabisa. Ubinadamu Wake wa kawaida ulikuwa uthibitisho kuwa Mungu Alipata mwili, na kwamba Enzi ya Neema ilikuwa enzi ya kazi ya Mungu mwenye mwili, si enzi ya kazi ya Roho. Ilikuwa uthibitisho kuwa Roho wa Mungu Alipatikana kikamilifu katika mwili, kwamba katika enzi ya kupata mwili kwa Mungu mwili Wake ungetekeleza kazi yote ya Roho. Kristo mwenye ubinadamu wa kawaida ni mwili ambao kwao Roho Hupatikana, Akiwa na ubinadamu wa kawaida, ufahamu wa kawaida, na fikira za wanadamu. “Kupatikana” kunamaanisha Mungu kuwa mwanadamu, Roho kuwa

mwili; kuiweka wazi, ni wakati ambapo Mungu Mwenyewe Anaishi katika mwili wenye ubinadamu wa kawaida, na kupitia kwenye huo mwili, Anaonyesha kazi yake ya uungu—hii ndiyo maana ya kupatikana, au kupata mwili. Wakati wa kupata mwili Kwake mara ya kwanza, ilikuwa muhimu kwa Mungu kuponya wagonjwa na kufukuza mapepo kwa sababu kazi Yake ilikuwa ni kukomboa. Ili kulikomboa kabila lote la mwanadamu, Alipaswa kuwa mwenye upendo na mwenye kusamehe. Kazi Aliyoifanya kabla ya kusulubiwa ilikuwa kuponya watu na kufukuza mapepo, ambayo iliashiria wokovu Wake wa mwanadamu kutoka katika dhambi na uchafu. Kwa sababu ilikuwa ni Enzi ya Neema, ilikuwa muhimu Kwake kuponya wagonjwa, na kwa njia hiyo Alionyesha ishara na miujiza, mambo ambayo yalikuwa kiwakilishi cha neema katika hiyo enzi; kwani Enzi ya Neema ilikitwa katika kutolewa kwa neema, ikiashiriwa na amani, furaha, na baraka ya vitu, vyote vikiwa zawadi za imani ya watu kwa Yesu. Hii ni kusema kuwa, kuponya wagonjwa, kufukuza mapepo na kutoa neema ulikuwa uwezo asilia wa mwili wa Yesu katika Enzi ya Neema, mambo haya yalikuwa ni kazi ya Roho iliyopatikana katika mwili. Lakini Alipokuwa Akitekeleza kazi kama hiyo, Alikuwa Akiishi katika mwili, Hakuenda nje ya mipaka ya mwili. Haijalishi ni matendo gani ya uponyaji Aliyotekeleza, bado Alikuwa na ubinadamu wa kawaida, bado Aliishi maisha ya kawaida ya binadamu. Sababu inayonifanya Niseme kuwa katika enzi ya kupata mwili kwa Mungu mwili ulitekeleza kazi yote ya Roho, ni kuwa haijalishi ni kazi gani Aliyoifanya, Aliifanya katika mwili. Lakini kwa sababu ya kazi Yake, watu hawakuchulia mwili Wake kuwa ulikuwa na kiini cha kimwili, kwani huu mwili ungefanya maajabu, na baadhi ya nyakati maalum ungefanya mambo ambayo yalivuka uwezo wa kimwili. Kwa hakika, haya matukio yote yalitokea Alipoanza huduma Yake, kama vile Yeye kujaribiwa kwa siku arobaini au kubadilishwa kule mlimani. Hivyo kwa Yesu, maana ya kupata mwili kwa Mungu haikukamilishwa, ila tu sehemu yake ilitimizwa. Maisha Aliyoishi katika mwili kabla ya kuanza kazi Yake yalikuwa ya kawaida tu katika hali zote. Alipoanza kazi Alidumisha umbo la nje la mwili Wake tu. Kwa sababu kazi Yake ilikuwa onyesho la uungu Wake, ilipita kazi ya kawaida ya mwili. Hata hivyo, Mwili wa Mungu ulikuwa tofauti na wanadamu wenye nyama na damu. Kwa hakika, katika maisha Yake ya kila siku, Alihitaji chakula, nguo, usingizi, na makao kama mtu yeyote yule, Alikuwa na mahitaji ya lazima ya kawaida, Alifikiri na kuwaza kama mwanadamu wa kawaida. Bado watu walimchukulia kuwa mwanadamu wa kawaida, isipokuwa tu kwamba kazi Aliyoifanya ilikuwa ya kupita akili. Kwa hakika, haijalishi Alifanya nini, Aliishi katika ubinadamu wa kawaida, na hata Alipotekeleza kazi, fikira zake zilikuwa za kawaida, mawazo yake yalikuwa ya wazi, hata zaidi ya wanadamu wa kawaida. Ilikuwa muhimu kwa Mungu mwenye mwili kufikiri kwa njia hii, kwani kazi ya uungu ilipaswa ionyeshwe na mwili ambao fikira zake zilikuwa za kawaida sana na mawazo yake wazi kabisa—ni kwa njia hii tu ndiyo mwili Wake ungeweza kuonyesha kazi ya uungu. Wakati wote wa miaka yote thelathini na tatu na nusu ambayo Yesu Aliishi duniani, Alidumisha

ubinadamu Wake wa Kawaida, ila kwa sababu ya kazi Yake katika huduma Yake ya miaka mitatu na nusu, watu walidhani kuwa Alikuwa Amepita mipaka ya ubinadamu, kwamba Alikuwa wa rohani zaidi kuliko hapo awali. Kwa kweli, ubinadamu wa kawaida wa Yesu haukubadilika kabla na baada ya Yeye kuanza huduma Yake; ubinadamu Wake ulikuwa sawa wakati wote, lakini kwa sababu ya tofauti kabla na baada ya Yeye kuanza huduma Yake, mitazamo miwili ilijitokeza kuhusiana na mwili Wake. Haijalishi watu walifikiria nini, Mungu mwenye mwili Alidumisha ubinadamu Wake asilia wa kawaida kipindi chote, kwani kwa sababu Mungu Alikuwa mwili, Aliishi katika mwili, mwili uliokuwa na ubinadamu wa kawaida. Hata ikiwa Alikuwa Anatekeleza huduma Yake au la, ubinadamu Wake wa kawaida usingeweza kufutika, kwani ubinadamu ndio kiini cha msingi cha mwili. Kabla Yesu hajaanza kutekeleza huduma Yake, mwili Wake ulibaki wa kawaida kabisa, ukishiriki katika shughuli zote za binadamu; Hakuonekana hata kidogo kuwa wa rohani, Hakuonyesha ishara zozote za kimiujiza. Wakati ule Alikuwa tu mwanadamu wa kawaida sana Aliyemwabudu Mungu, japo dhamira Yake ilikuwa adilifu sana, ya kweli zaidi kuliko ya mtu yeyote. Hivi ndivyo ubinadamu Wake wa kawaida ulijionyesha wenyewe. Kwa kuwa Hakufanya kazi kabisa kabla ya kuianza huduma Yake, hakuna aliyemtambua, hakuna aliyegundua kuwa mwili Wake ulikuwa tofauti kabisa na miili ya watu wengine, kwa kuwa Hakutenda muujiza hata mmoja, Hakutenda hata chembe ya Kazi ya Mungu. Hata hivyo, baada ya kuanza kutekeleza kazi Yake, Alidumisha umbo la nje la ubinadamu wa kawaida na kuendelea kuishi katika mawazo ya kawaida ya binadamu, lakini kwa kuwa Alikuwa Ameanza kufanya kazi ya Mungu Mwenyewe, kuanzisha huduma ya Kristo na kufanya kazi ambayo wanadamu hai, wanadamu wenye nyama na damu, wasingeweza kufanya, basi watu walidhani kuwa Hakuwa na ubinadamu wa kawaida na Hakuwa mwili wa kawaida kikamilifu ila mwili usio kamili. Kwa sababu ya yale Aliyotekeleza, watu walisema kuwa Alikuwa Mungu katika mwili Ambaye Hakuwa na ubinadamu wa kawaida. Huu ulikuwa ufahamu wa kimakosa, kwani watu hawakuelewa maana ya Mungu kupata mwili. Huu ufahamu mbaya ulitokana na ukweli kuwa kazi iliyoonyeshwa na Mungu katika mwili ilikuwa kazi ya uungu, iliyoonyeshwa kupitia kwa mwili wenye ubinadamu wa kawaida. Mungu Alikuwa Amevishwa katika mwili, Alikaa ndani ya mwili, na kazi Yake katika ubinadamu Wake iliuziba ukawaida wa ubinadamu Wake. Kwa sababu hii, watu walidhani kuwa Mungu hakuwa na ubinadamu bali uungu tu.

Mungu katika kupata mwili Kwake mara ya kwanza Hakukamilisha kazi ya kupata mwili; Alikamilisha tu hatua ya kwanza ya kazi iliyokuwa lazima kwa Mungu kuifanya katika mwili. Kwa hivyo, ili kuimaliza kazi ya kupata mwili, Mungu Amerudi katika mwili kwa mara nyingine tena, Akiishi kulingana na ukawaida na uhalisia wote wa mwili, yaani, kuifanya kazi ya Mungu ijitokeze katika mwili wa kawaida kabisa, na kwa njia hiyo Anahitimisha kazi Aliyoiacha bila

kukamilisha katika mwili. Mwili wa pili uliopatikana kimsingi ni sawa na ule wa kwanza, lakini ni halisi zaidi, wa kawaida kabisa kuliko ule wa kwanza. Kwa sababu hiyo, mateso unayoyapitia mwili wa pili uliopatikana ni makubwa kuliko yale ya ule wa kwanza, ila mateso haya ni kwa sababu ya huduma Yake katika mwili, ambayo ni tofauti na mateso ya mwanadamu mwovu. Vilevile yanachipuka kutokana na ukawaida na uhalisi wa mwili Wake. Kwa kuwa Anatekeleza huduma Yake katika mwili wa kawaida na halisi kabisa, mwili ni sharti upitie mateso mazito. Kadiri mwili ulivyo wa kawaida na halisi, ndivyo unateseka zaidi katika utekelezaji wa huduma Yake. Kazi ya Mungu inaonyeshwa katika mwili wa kawaida sana, mwili ambao si wa rohoni kamwe. Kwa kuwa mwili Wake ni wa kawaida, na ni lazima ubebe kazi ya kumwokoza mwanadamu, Anateseka hata zaidi kuliko ambavyo mwili wa rohoni unaweza kuteseka—mateso haya yote yanatokana na uhalisi na ukawaida wa mwili Wake. Kutokana na mateso yaliyopitiwa na hii miili miwili iliyopatikana wakati wa kutekeleza huduma Zao, mtu anaweza kuona kiini cha mwili uliopatikana. Kadiri mwili ulivyo wa kawaida, ndivyo Anapata mateso mazito. Afanyapo kazi, kadiri mwili unaofanya kazi unavyokuwa wa kweli, ndivyo maoni ya watu yanaendelea kuwa makali, na hatari zinazomkabili zinaendelea kuongezeka. Lakini, kadiri mwili ulivyo halisi, kadiri mwili unavyokuwa na hali kamili ya binadamu wa kawaida, ndivyo Anaweza zaidi kuifanya kazi ya Mungu katika mwili. Ulikuwa mwili wa Yesu ulioangikwa msalabani, mwili Wake Alioutoa kama kafara kwa dhambi; ni kupitia kwa mwili wenye ubinadamu wa kawaida ndipo Aliweza kumshinda Shetani na kumkomboa kabisa mwanadamu kutoka msalabani. Ni kupitia mwili kamili ndipo Mungu katika mwili mara ya pili Anatekeleza kazi ya ushindi na kumshinda Shetani. Ni mwili tu wa kawaida na halisi kabisa unaoweza kutekeleza kazi ya ushindi kwa ukamilifu wake na kutoa ushuhuda wa nguvu. Hii ni sawa na kusema kwamba ushindi juu ya mwanadamu inafanywa kuwa bora kupitia uhalisia na ukawaida wa mwili wa Mungu, si kupitia miujiza mikuu na ufunuo. Huduma ya huyu Mungu mwenye mwili ni ya kunena na kwa njia hiyo inamshinda mwanadamu na kumfanya mkamilifu; kwa maneno mengine, kazi ya Roho Aliyejitokeza katika mwili, wajibu wa mwili, ni kunena na kupitia kwa hili kumshinda, kumfichua, kumfanya kuwa kamilifu, na kumwondoa mwanadamu kabisa. Kwa hivyo, ni katika kazi ya kushinda ambapo kazi ya Mungu katika mwili itatimizwa kwa ukamilifu. Kazi ya ukombozi ya kwanza ilikuwa mwanzo tu wa kazi ya kupata mwili kwa Yesu; mwili unaofanya kazi ya kushinda utakamilisha kazi nzima ya kupata mwili kwa Yesu. Kijinsia, mmoja ni mwanamke na mwingine ni mwanamume; kwa hili, maana ya kupata mwili kwa Mungu imekamilishwa. Mawazo mabaya ya mwanadamu kumhusu Mungu yameondolewa: Mungu Anaweza kuwa mwanamke na mwanamume, na kimsingi Mungu mwenye mwili Hana jinsia. Alimuumba mwanamume na mwanamke, na Kwake, hakuna mgawanyiko wa jinsia. Katika hatua hii ya kazi, Mungu Hafanyi ishara na miujiza, ili kwamba kazi iweze kutimiza matokeo yake kupitia kwa maneno. Sababu ya jambo hili, aidha, ni kwa maana kazi ya Mungu

mwenye mwili mara hii si kuponya wagonjwa na kufukuza mapepo, ila kumshinda mwanadamu kupitia kunena, ikiwa na maana kwamba uwezo asili uliomo kwenye huu mwili uliopatikana wa Mungu ni kunena maneno na kumshinda mwanadamu, si kuponya wagonjwa na kufukuza mapepo. Kazi Yake katika ubinadamu wa kawaida si kutenda miujiza, si kuponya wagonjwa na kufukuza mapepo, ila ni kunena, na kwa hivyo Yesu kupata mwili kwa mara ya pili kunaonekana kwa watu kuwa kawaida zaidi ya mara ya kwanza. Watu wanaona kuwa Mungu kupata mwili si uongo; lakini huyu Mungu mwenye mwili ni tofauti na Yesu Aliyekuwa mwili, na japo wote ni Mungu wenye mwili, Hawako sawa kabisa. Yesu Alikuwa na ubinadamu wa desturi, ubinadamu wa kawaida, lakini Aliambatana na ishara nyingi na miujiza. Katika huyu Mungu mwenye mwili, macho ya mwanadamu hayataona ishara au miujiza, wala kuponya wagonjwa au kufukuza mapepo, wala kutembea juu ya bahari, wala kufunga kwa siku arobaini... Hafanyi kazi sawa na Aliyoifanya Yesu, si kwa kuwa mwili Wake kimsingi ni tofauti na ule wa Yesu, ila ni kwa sababu si huduma Yake kuponya wagonjwa na kufukuza mapepo. Haharibu kazi Yake mwenyewe, Havurugi kazi Yake mwenyewe. Kwa kuwa anamshinda mwanadamu kwa maneno Yake halisi, haina haja ya kumhini kwa miujiza, na kwa hivyo hii hatua ni kukamilisha kazi ya kupata mwili. Mungu mwenye mwili umwonaye leo ni mwili kabisa, na hana hali ya rohani ndani yake. Anakuwa mgonjwa sawa tu na watu wengine, Anahitaji chakula na nguo sawa tu na watu wengine, kwani ni mwili kabisa. Ikiwa wakati huu Mungu mwenye mwili Angetekeleza ishara na miujiza mikuu, ikiwa Angeponya wagonjwa, kufukuza mapepo, au Angeweza kuua kwa neno moja tu, kazi ya kushinda ingefanywaje? Kazi ingeenezwa vipi miongoni mwa watu wa Mataifa? Kuponya wagonjwa na kufukuza mapepo ilikuwa kazi ya Enzi ya Neema, hatua ya kwanza katika kazi ya ukombozi, na sasa kwa kuwa Mungu Amemkomboa mwanadamu kutoka msalabani, Hatekelezi kazi hiyo kamwe. Ikiwa katika siku za mwisho “Mungu” sawa na Yesu Angeonekana, Ambaye Anaponya wagonjwa, Anafukuza mapepo na Anayesulubiwa kwa ajili ya wanadamu, “Mungu” huyo, japo Analingana na maelezo ya Mungu katika Biblia, na rahisi kwa mwanadamu kukubali, Hangeweza, katika kiini chake, kuwa mwili uliovaliwa na Roho wa Mungu, bali na roho mwovu. Kwani ni kanuni ya kazi ya Mungu kutorudia Alichokikamilisha. Hivyo basi kazi ya kupata mwili wa Mungu kwa mara ya pili ni tofauti na kule kwa kwanza. Katika siku za mwisho, Mungu Anafanikisha kazi ya kushinda katika mwili wa kawaida; Haponyi wagonjwa, Hatasulubishwa kwa ajili ya mwanadamu, ila tu Ananena maneno katika mwili, Anamshinda mwanadamu katika mwili. Ni mwili kama huo tu ndio mwili wa Mungu katika mwili; ni mwili kama huo tu ndio unaoweza kukamilisha Kazi ya Mungu katika mwili.

Ikiwa katika hii hatua Mungu mwenye mwili Anapitia ugumu au Anatekeleza huduma Yake, Anafanya hivyo ili kukamilisha maana ya kupata mwili, kwani huku ndiko Mungu kupata mwili kwa mara ya mwisho. Mungu Anaweza kuwa mwili mara mbili tu. Hakuwezi kuwepo

mara ya tatu. Kuwa mwili kwa mara ya kwanza Alikuwa ni wa kiume, wa pili ni wa kike, na kwa hivyo sura ya mwili wa Mungu imekamiliwa katika akili za mwanadamu; aidha, huku kuwa mwili mara mbili tayari kumemaliza kazi ya Mungu katika mwili. Mara ya kwanza, Mungu mwenye mwili Alikuwa na ubinadamu wa kawaida, ili kukamilisha maana ya kupata mwili. Mara hii vilevile Ana ubinadamu wa kawaida ila maana ya huku kupata mwili ni tofauti: ni kwa kina, na kazi Yake ni ya umuhimu mkubwa. Sababu ya Mungu kuwa mwili tena ni kukamilisha maana ya kupata mwili. Mungu Akiikamilisha kabisa hii hatua ya kazi Yake, maana nzima ya kupata mwili, yaani, kazi ya Mungu katika mwili, itakuwa imekamiliwa, na hakutakuwa na kazi nyingine ya kufanywa katika mwili. Yaani, tangu sasa Mungu Hatawahi tena kuja katika mwili kufanya kazi Yake. Ni kwa kuokoa na kumfanya mwanadamu kuwa mkamilifu pekee ndiko Mungu Hufanya kazi ya kupata mwili. Kwa maneno mengine, si jambo la kawaida kwa Mungu kuwa na mwili, ila tu ni kwa minajili ya kazi. Kwa kuja kufanya kazi Akiwa kwenye mwili, Anamwonyesha Shetani kuwa Mungu ni mwili, mtu wa kawaida—lakini Anaweza kuitawala dunia kwa ushindi, Anaweza kumshinda Shetani, kumkomboa mwanadamu na kumshinda mwanadamu! Lengo la kazi ya Shetani ni kuwapotosha wanadamu, ilhali lengo la Mungu ni kuwaokoa wanadamu. Shetani huwateka wanadamu katika shimo lisilo na mwisho, ilhali Mungu Huwaokoa kutoka humo shimoni. Shetani huwafanya wanadamu wote wamwabudu, ilhali Mungu Huwafanya wawe wafuasi wa utawala Wake, kwani Yeye ndiye Bwana wa viumbe wote. Kazi hii yote hutekelezwa kupitia Mungu kupata mwili mara mbili. Mwili Wake kimsingi ni muungano wa ubinadamu na uungu na huwa na ubinadamu wa kawaida. Kwa hivyo, bila Mungu kuwa mwili, Mungu Asingeweza kufikia matokeo katika ukombozi wa mwanadamu, na bila ubinadamu wa kawaida wa mwili Wake, kazi Yake katika mwili bado haingefikia matokeo. Kiini cha kupata mwili kwa Mungu ni kwamba lazima awe na ubinadamu wa kawaida; kwani ingekuwa vinginevyo, ingekuwa kinyume na madhumuni asili ya Mungu ya kupata mwili.

Kwa nini Ninasema kuwa maana ya kupata mwili haikukamilishwa katika kazi ya Yesu? Ni kwa sababu Neno halikuwa Mwili kikamilifu. Kilichofanywa na Yesu kilikuwa tu sehemu moja ya kazi ya Mungu katika mwili; Alifanya tu kazi ya ukombozi na Hakufanya kazi ya kumpata mwanadamu kikamilifu. Kwa sababu hii, Mungu Amekuwa mwili mara nyingine tena katika siku za mwisho. Hatua hii ya kazi, pia inafanywa katika mwili wa kawaida, ikifanywa na mwanadamu wa kawaida kabisa, ambaye ubinadamu wake haupiti mipaka ya ubinadamu. Kwa maneno mengine, Mungu Amekuwa mwanadamu kamili, na ni mtu ambaye utambulisho wake ni ule wa Mungu, mwanadamu kamili, mwili kamili, Ambaye Anatekeleza kazi. Katika jicho la mwanadamu, Yeye ni mwili tu ambao haujapita mipaka ya ubinadamu hata kidogo, mwanadamu wa kawaida kabisa Anayeweza kuzungumza lugha ya mbinguni, Ambaye Haonyeshi ishara za kimiujiza, Hafanyi miujiza, sembuse kuweka wazi ukweli wa ndani kuhusu dini katika kumbi

kuu za mikutano. Kazi ya kupata mwili kwa mara ya pili inaonekana kwa wanadamu kuwa tofauti kabisa na ile ya kwanza, kiasi kwamba kazi hizi mbili zinaonekana kutokuwa na uhusiano wowote, na hakuna chochote katika kazi ya kwanza kinachoweza kuonekana wakati huu. Japo kazi ya kupata mwili kwa mara ya pili ni tofauti na ile ya kwanza, hili halithibitishi kuwa chanzo Chao si kimoja na sawa. Iwapo chanzo Chao ni kimoja inategemea aina ya kazi iliyofanywa na miili na si katika maumbo Yao ya nje. Katika hatua tatu za kazi Yake, Mungu Amekuwa mwili mara mbili, na mara zote kazi ya Mungu kuwa mwili inaanzisha enzi mpya, inaanzisha kazi mpya; kuwa mwili kwa mara ya kwanza na pili kunakamilishana. Macho ya wanadamu hayawezi kugundua kuwa hii miili miwili kwa kweli imetokana na chanzo kimoja. Ni wazi kwamba hili liko nje ya uwezo wa macho ya wanadamu au akili za wanadamu. Ila katika kiini Chao, ni miili sawa, kwani kazi Yao inatokana na Roho mmoja. Iwapo hii miili miwili inatokana na chanzo kimoja haiwezi kuamuliwa kutokana na enzi na sehemu ilipozaliwa, au vigezo vingine kama hivyo, ila kwa kazi ya uungu iliyoonyeshwa Nayo. Kupata mwili wa pili hakufanyi kazi yoyote iliyofanywa na Yesu, kwani kazi ya Mungu haifuati makubaliano, lakini kila wakati inafungua njia mpya. Kupata mwili wa pili hakulengi kuongeza au kuimarisha maono ya kupata mwili wa kwanza katika akili za watu, ila kuutimiza na kuukamilisha, kuongeza kina cha wanadamu kumwelewa Mungu, kuvunja sheria zote ambazo zipo katika mioyo ya watu, na kufuta picha za uongo kuhusu Mungu mioyoni mwao. Ni wazi kuwa hakuna hatua yoyote ya kazi ya Mungu mwenyewe inaweza kumpa mwanadamu ufahamu kamili wa Mungu; kila mojawapo inatoa kwa sehemu tu, si ufahamu mzima. Japo Mungu Ameonyesha tabia Yake kikamilifu, kwa sababu ya upungufu wa ufahamu wa wanadamu, ufahamu wake kuhusu Mungu si kamili. Haiwezekani, kutumia lugha ya wanadamu, kueleza tabia nzima ya Mungu; basi hatua moja tu ya kazi Yake itamwelezaje Mungu kikamilifu? Anafanya kazi katika mwili kwa kujisetiri katika ubinadamu Wake wa kawaida, na mtu anaweza kumjua tu kupitia kwa maonyesho ya uungu Wake, si kupitia kwa umbo Lake la kimwili. Mungu Anakuja katika mwili kumruhusu mwanadamu Amjue kupitia kazi Zake mbalimbali, na hakuna hatua mbili za kazi Yake zinafanana. Ni kwa njia hii tu mwanadamu anaweza kuwa na ufahamu kamili wa kazi ya Mungu katika mwili, si kwa kujifunga katika kipengele kimoja tu. Japo kazi ya hii miili miwili iliyopatikana ni tofauti, kiini cha hii miili, na chanzo cha kazi Yao vinafanana; ni kwamba tu Ipo ili kutekeleza hatua mbili tofauti za kazi, na inatokea katika enzi mbili tofauti. Licha ya jambo lolote, miili ya Mungu katika mwili inashiriki kiini kimoja na asili moja—huu ni ukweli ambao hauwezi kupingwa na yeyote.

Kazi ya Mungu na Utendaji wa Mwanadamu

Kazi ya Mungu miongoni mwa mwanadamu haitengani na mwanadamu, kwa kuwa mwanadamu ni chombo cha kazi hii na kiumbe wa pekee aliyeumbwa na Mungu anayeweza

kutoa ushuhuda kwa Mungu. Maisha ya mwanadamu na shughuli zake zote havitengani na Mungu, na vyote vinaongozwa na mkono wa Mungu, na inaweza kusemwa kuwa hakuna mtu anayeweza kuishi bila Mungu. Hakuna anayeweza kupinga hili, kwani ndio ukweli. Kila Akifanyacho Mungu ni kwa faida ya mwanadamu, na kinalenga hila za Shetani. Kila anachokihitaji mwanadamu kinatoka kwa Mungu, na Mungu ndiye chanzo cha maisha ya mwanadamu. Hivyo basi, mwanadamu hana uwezo wa kujitenga na Mungu. Vilevile, Mungu Hajawahi kuwa na nia ya kujitenga na mwanadamu. Kazi Aifanyayo Mungu ni kwa ajili ya wanadamu wote na mawazo Yake daima ni mema. Kwa mwanadamu, kwa hivyo, kazi ya Mungu na mawazo ya Mungu kwa mwanadamu (yaani mapenzi ya Mungu) ni “maono” ambayo yanafaa kutambuliwa na mwanadamu. Maono kama hayo pia ni usimamizi wa Mungu, na kazi ambayo haiwezi kufanywa na mwanadamu. Mahitaji ambayo Mungu anatarajia kutoka kwa mwanadamu wakati wa kazi Yake, wakati uo huo, yanaitwa “vitendo” vya mwanadamu. Maono ni kazi ya Mungu Mwenyewe au ni mapenzi Yake kwa mwanadamu au madhumuni na umuhimu wa kazi Yake. Maono pia yanaweza kusemekana kuwa sehemu ya usimamizi, kwani usimamizi huu ni kazi ya Mungu, iliyokusudiwa kwa mwanadamu, kwa maana kwamba ni kazi ambayo Mungu anaifanya miongoni mwa wanadamu. Kazi hii ni ushahidi na njia ambayo kwayo mwanadamu anamfahamu Mungu na ni ya umuhimu wa hali ya juu kwa mwanadamu. Iwapo wanadamu hawatatilia maanani kuijua kazi ya Mungu na badala yake kutilia maanani mafundisho ya dini kuhusu imani kwa Mungu au kutilia maanani vitu vidogo visivyo na maana, hawatamjua Mungu, na, aidha, hawatakuwa wanautafuta moyo wa Mungu. Kazi ya Mungu inamsaidia sana mwanadamu kumfahamu Mungu na inaitwa maono. Maono haya ni kazi ya Mungu, mapenzi, madhumuni na umuhimu wa kazi ya Mungu na yote ni kwa manufaa ya mwanadamu. Vitendo vinamaanisha yale ambayo yanafaa kufanywa na mwanadamu, yale ambayo yanafaa yafanywe na viumbe wanaomfuata Mungu. Ni wajibu wa mwanadamu pia. Kinachotakiwa kufanywa na mwanadamu si kile alichokielewa tangu awali bali ni yale matakwa ya Mungu wakati wa kuifanya kazi Yake. Matakwa haya taratibu yanakuwa ya kina na kuinuliwa kadri Mungu anavyofanya kazi. Kwa mfano, katika Enzi ya Sheria, mwanadamu alilazimika kuifuata sheria na katika Enzi ya Neema mwanadamu alitakiwa kuubeba msalaba. Enzi ya Ufalme ni tofauti: Matakwa kwa mwanadamu ni mazito kuliko yale ya Enzi ya Sheria na Enzi ya Neema. Kadiri maono yanavyoinuliwa zaidi ndivyo matakwa haya yanavyokuwa mazito, ya wazi zaidi na halisi. Vivyo hivyo, maono yanaendelea kuwa halisi. Maono haya mengi na halisi si fursa tu ya utiifu wa mwanadamu kwa Mungu, bali pia, zaidi ya hayo, yanamsaidia yeye kumfahamu Mungu.

Ikilinganishwa na enzi za awali, kazi ya Mungu katika Enzi ya Ufalme ni ya vitendo zaidi, imekusudiwa zaidi dutu ya mwanadamu na mabadiliko katika tabia yake na uwezo zaidi wa

kuwa na ushuhuda wa Mungu Mwenyewe kwa wale wote wamfuatao Mungu. Kwa maneno mengine, katika Enzi ya Ufalme, Mungu anapofanya kazi hujionyesha zaidi kwa mwanadamu, kuliko kipindi kingine chochote kile cha awali, ikiwa inamaanisha kuwa maono ambayo yanafaa kujulikana na mwanadamu ni ya juu kuliko yale ya enzi yoyote ile ya awali. Kwa kuwa kazi ya Mungu miongoni mwa mwanadamu imeingia maeneo ambayo haikuwa imefika, maono yanayojulikana na mwanadamu katika Enzi ya Ufalme ni ya juu zaidi katika kazi nzima ya usimamizi. Kazi ya Mungu imeingia katika maeneo ambayo haikuwa imewahi kufika, na kwa hivyo maono yanayojulikana na mwanadamu yamekuwa ya juu zaidi katika maono yote, na matokeo ya vitendo vya mwanadamu ni ya juu zaidi kuliko enzi za awali kwani utendaji wa mwanadamu hubadilika kulingana na mabadiliko ya maono na ukamilifu wa maono vilevile huonyesha ukamilifu wa vitendo vya mwanadamu. Punde tu usimamizi wa Mungu usitapo, vitendo vya mwanadamu navyo husimama, na bila kazi ya Mungu mwanadamu hatakuwa na jingine ila tu kujikita katika mafundisho ya zamani, vinginevyo hatakuwa na pa kukimbilia. Bila maono mapya, hapatakuwa na utendaji mpya kutoka kwa mwanadamu; bila kuwepo na maono kamili hapatakuwa na utendaji kamili wa mwanadamu; na bila maono ya juu hapatakuwa na utendaji wa juu wa mwanadamu. Utendaji wa mwanadamu huandamana na nyayo za Mungu na vivyo hivyo ufahamu na tajriba ya mwanadamu hubadilika sawa na kazi ya Mungu. Bila kujali mwanadamu ana uwezo kiasi gani, hawezi kujitenga na Mungu, na iwapo Mungu angaliacha kufanya kazi hata kwa muda kidogo, mwanadamu angalikufa ghafla kutokana na ghadhabu ya Mungu. Mwanadamu hana lolote la kujivunia, kwani haijalishi ufahamu wa mwanadamu ulivyo wa juu leo, haijalishi jinsi uzoefu wake ulivyo wa kina, hawezi kujitenga na kazi ya Mungu—kwani vitendo vya mwanadamu na yale yote anayoyaandama katika imani yake kwa Mungu, hayatengani na maono haya. Katika tukio la kazi ya Mungu, kuna maono ambayo mwanadami anapaswa kujua, na, kufuatia haya matarajio mwafaka huwekewa mwanadamu. Bila haya maono kama msingi, mwanadamu hawezi kuwa na uwezo wa utendaji na pia hangeweza kumfuata Mungu bila kuyumbayumba. Ikiwa mwanadamu hamjui Mungu au hayaalewi mapenzi ya Mungu, basi yote ayafanyayo ni bure na yasiyoweza kukubalika na Mungu. Hata mwanadamu awe na vipawa vingi kiasi gani, bado hawezi kujitenga na kazi ya Mungu na uongozi wa Mungu. Bila kujali uzuri na wingi wa matendo ya mwanadamu, bado hayawezi kuchukua nafasi ya kazi ya Mungu. Kwa hivyo basi, utendaji wa mwanadamu hauwezi kutenganishwa na maono katika hali yoyote ile. Wale ambao hawakubali maono mapya hawana vitendo vipya. Vitendo vyao havina uhusiano na ukweli kwani wanajifunga katika mafundisho ya dini na kufuata sheria zilizokufa; hawana maono mapya kabisa na kwa sababu hiyo hawatendi kulingana na enzi mpya. Wamepoteza maono na kwa kufanya hivyo wamepoteza kazi ya Roho Mtakatifu, hivyo basi kupoteza ukweli pia. Wasio na ukweli ni wazawa wa upuuzi, ni mifano ya Shetani. Bila kujali mtu ni wa aina gani, hawezi kuwepo bila maono ya kazi ya Mungu, hawezi kuishi pasipo na

uwepo wa Roho Mtakatifu; punde tu mtu apotezapo maono, anaingia Kuzimu na kuishi gizani. Watu wasio na maono ni wale wamfuatao Mungu kipumbavu, ni wale wasio na kazi ya Roho Mtakatifu, na wanaishi kuzimu. Watu kama hawa huwa hawafuatilii ukweli, na hilitundika jina la Mungu kama bango. Wale ambao hawafahamu kazi ya Roho Mtakatifu, ambao hawamjui Mungu katika mwili, ambao hawajui hatua tatu za kazi katika uzima wa usimamizi wa Mungu—hawajui maono na hivyo wanaishi bila ukweli. Je, si wale wote wasiokuwa na ukweli ni watenda maovu? Wale wanaotaka kuweka ukweli katika vitendo, ambao wako tayari kuutafuta ufahamu wa Mungu, na ambao kwa kweli wanashirikiana na Mungu ni watu ambao maono yanakuwa msingi wao. Wanakubaliwa na Mungu kwa sababu wanashirikiana na Mungu na ushirika huu ndio ambao unafaa kuwekwa katika vitendo na mwanadamu.

Katika maono kuna njia nyingi zinazoelekea kwa vitendo. Matakwa ya utendaji yaliyopo kwa mwanadamu yamo pia ndani ya maono sawa tu na kazi ya Mungu inayopaswa kufahamika na mwanadamu. Katika mikutano maalum ya zamani au mikutano mikuu iliyokuwa katika sehemu mbalimbali, ni kipengele kimoja tu cha vitendo kilichozungumziwa. Vitendo kama hivyo ni vile vilivyotiwa katika vitendo katika Enzi ya Neema na hapakuwa na mfanano wowote na ufahamu wa Mungu kwani maono ya Enzi ya Neema yalikuwa tu maono ya kusulubiwa kwa Yesu, na hapakuwa na maono ya juu zaidi. Mwanadamu hakuhitajika kujua zaidi ya kazi Yake ya ukombozi wa mwanadamu kupitia kusulubiwa, na kwa hivyo katika Enzi ya Neema hapakuwa na maono mengine ya kufahamiwa na mwanadamu. Kwa njia hii, mwanadamu alikuwa na ufahamu mdogo sana wa Mungu na mbali na upendo na huruma za Yesu, kulikuwa na vitu vichache tu vya mwanadamu kuweka katika vitendo, vitu ambavyo vilikuwa tofauti na hali ya leo. Zamani, haikujalisha mkutano wake ulichukua umbo lipi, mwanadamu hakuwa na uwezo wa kuzungumzia ufahamu wa vitendo wa kazi ya Mungu, sembuse kuwepo na yeyote aliyeweza kusema kwa dhahiri njia iliyokuwa sawa ya utendaji kwa mwanadamu kuiingilia. Mwanadamu aliongeza tu mambo kidogo katika msingi wa stahamala na uvumilivu; hapakuwa na mabadiliko yoyote katika kiini cha vitendo vyake kwani katika enzi hiyo Mungu hakufanya kazi yoyote mpya na matakwa ya pekee Aliyomwekea mwanadamu yalikuwa stahamala na uvumilivu, au kuubeba msalaba. Mbali na vitendo kama hivyo, hapakuwa na maono ya juu zaidi kuliko yale ya kusulubishwa kwa Yesu. Zamani hapakutajwa maono mengine kwa sababu Mungu hakufanya kazi kubwa na kwa sababu Alimwekea mwanadamu matakwa machache. Kwa njia hii, haikujalisha mwanadamu alifanya nini, hakuweza kuivuka mipaka ya viwango hivi, viwango ambavyo vilikuwa rahisi na vya juu juu vya mwanadamu kuweka katika vitendo. Leo Nazungumzia maono mengine kwa kuwa leo kazi nyingi zaidi imefanywa, kazi ambayo ni mara kadha zaidi ya ile ya Enzi ya Sheria na Enzi ya Neema. Yanayohitajika kwa mwanadamu, aidha, ni mara kadhaa juu zaidi kuliko enzi zilizopita. Iwapo mwanadamu hana uwezo wa kuijua

kikamilifu kazi kama hiyo, basi haitakuwa na umuhimu mkubwa; inaweza kuchukuliwa kuwa mwanadamu atakuwa na ugumu kuifahamu kazi yenyewe kikamilifu ikiwa hawezi kuitengea maisha yake yote. Katika kazi ya ushindi, kuzungumzia tu njia ya vitendo kutaufanya ushindi wa mwanadamu kuwa jambo lisilowezekana. Mazungumzo ya maono tu bila matakwa yoyote kwa mwanadamu vilevile kutaufanya ushindi wa mwanadamu kuwa jambo lisilowezekana. Iwapo hapana kitu kingine kitakachoweza kuzungumziwa ila tu njia ya vitendo, basi ingekuwa vigumu kuuweza udhaifu wa mwanadamu, au kuondoa dhana za mwanadamu, na vilevile itakuwa vigumu kumshinda mwanadamu. Maono ni zana muhimu ya ushindi wa mwanadamu, na bado pasingelikuwepo na njia ya vitendo tofauti na maono basi mwanadamu asingelikuwa na njia ya kufuata wala jinsi ya kuingia. Hii imekuwa kanuni ya kazi ya Mungu toka mwanzo hadi mwisho: Katika maono kuna kile ambacho chaweza kuwekwa katika vitendo, na vivyo hivyo kuna maono kuongezea kwa kutenda. Kiwango cha mabadiliko katika maisha na tabia za mwanadamu huambatana na mabadiliko katika maono. Kama mwanadamu angetegemea tu juhudi zake, basi ingekuwa vigumu kwake kufikia kiwango cha juu cha mabadiliko. Maono huzungumzia kazi ya Mungu Mwenyewe na usimamizi wa Mungu. Utendaji hurejelea njia ya vitendo vya mwanadamu na kwa namna ya maisha ya mwanadamu; katika usimamizi wote wa Mungu, uhusiano baina ya maono na vitendo ni uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Maono yangetolewa au yangezungumziwa bila kuhusishwa na vitendo, ama kungekuwa tu na maono na vitendo vya mwanadamu viondolewe, basi vitu kama hivyo visingechukuliwa kama usimamizi wa Mungu, wala isingesemwa kwamba kazi ya Mungu ni kwa ajili ya wanadamu; kwa namna hii, si tu kwamba wajibu wa mwanadamu ungeondolewa, bali pia kazi ya Mungu ingekosa kusudi. Iwapo tangu mwanzo hadi mwisho, mwanadamu angetarajiwa tu kutenda, bila kujihusisha na kazi ya Mungu, na, zaidi ya hayo, kama mwanadamu asingetarajiwa kuifahamu kazi ya Mungu, basi kazi hiyo isingelitwa usimamizi wa Mungu. Kama mwanadamu hangemjua Mungu, na hangejua mapenzi ya Mungu, na huendelea kufanya vitendo kidhahania bila kuwa na uwazi, basi asingekuwa kiumbe kilichohitimu. Hivyo basi, hivi vitu viwili ni vya lazima. Kama kungekuwepo kazi ya Mungu tu, ambayo ni kusema, kungekuwepo maono pekee na hakungekuwepo na ushirikiano au vitendo kutoka kwa mwanadamu, basi hivyo vitu visingelitwa usimamizi wa Mungu. Iwapo kungekuwa tu na vitendo na kuingia kwa mwanadamu, basi bila kujali kuingia kwa mtu kungekuwa kwa juu kiasi gani, haya, pia, hayangekubalika. Kuingia kwa mwanadamu kunafaa kubadilika taratibu kulingana na kazi na maono; hakuwezi kubadilika ghafla. Kanuni za vitendo vya mwanadamu haziko huru na bila vizuizi, lakini ziko ndani ya mipaka fulani. Kanuni hizo hubadilika kwa hatua sawa na maono ya kazi. Hivyo basi usimamizi wa Mungu hatimaye huishia katika kazi ya Mungu na vitendo vya mwanadamu.

Kazi ya usimamizi ilikuja tu kwa ajili ya wanadamu, yaani ilitolewa kwa ajili ya uwepo wa

wanadamu. Usimamizi haukuwepo kabla ya uwepo wa wanadamu au mwanzo wakati mbingu na nchi na vilivyomo vilipoumbwa. Iwapo, katika kazi nzima ya Mungu, hakungekuwa na vitendo vinavyomfaidi mwanadamu, yaani kama Mungu asingeweka matakwa maalum kwa mwanadamu aliyepotoka (ikiwa kazi ifanywayo na Mungu haikuwa na njia nzuri ya vitendo vya mwanaadamu), basi kazi hii isingelitwa usimamizi wa Mungu. Iwapo kazi nzima ya Mungu ingehusisha tu kuwaambia wanadamu waliopotoka jinsi ya kuendeleza vitendo vyao, na Mungu hakuendeleza kazi yoyote ya mipango Yake, na Hakuonyesha uwepo wake wa daima au busara, basi bila kujali ni jinsi gani matakwa ya Mungu kwa mwanadamu yangewekwa juu, bila kujali Mungu aliishi muda mrefu kiasi gani miongoni mwa wanadamu, mwanadamu asingejua chochote juu ya tabia ya Mungu; kama ingekuwa hivyo, basi kazi hii isingeweza kukaribia kuitwa usimamizi wa Mungu. Kwa ufupi, kazi ya usimamizi wa Mungu ni kazi iliyofanywa na Mungu na kazi zote zilizofanywa chini ya uongozi wa Mungu na wale ambao wamepatikana na Mungu. Kazi kama hiyo inaweza kuchukuliwa kwa ufupisho kama usimamizi. Kwa maneno mengine, kazi ya Mungu miongoni mwa wanadamu na vilevile ni ushirikiano Wake na wale wanaomfuata kwa ujumla yanaitwa usimamizi. Hapa kazi ya Mungu inaitwa maono na ushirikiano wa mwanadamu unaitwa vitendo. Kadiri kazi ya Mungu ilivyo juu (yaani kadiri maono yalivyo juu), ndivyo tabia za Mungu zinakuwa wazi kwa mwanadamu, na kutoafikiana na mawazo ya mwanadamu, na ndivyo vitendo na ushirikiano wa mwanadamu huwa vya juu. Kadiri matakwa kwa mwanadamu yanavyokuwa ya juu, ndivyo kazi ya Mungu inavyotofautiana mawazo ya mwanadamu, matokeo yake yakiwa majaribu ya mwanadamu, na viwango anavyotarajiwa kuwa navyo, vilevile vinakuwa vya juu. Katika hatima ya kazi hii, maono yote yatakuwa yametimizwa, na yale yote mwanadamu anapaswa kuweka katika vitendo yatakuwa yamefikia kilele cha ukamilifu. Huu ndio wakati pia ambapo kila kitu kitawekwa katika kundi lake kwani kile kinachopaswa kufahamika na mwanadamu kitakuwa kimebainishwa kwake. Kwa hivyo maono yatakapofikia upeo wa juu, vivyo hivyo kazi nayo itakaribia hatima yake na vitendo vya mwanadamu vitakuwa vimefikia ufanisi wake. Vitendo vya mwanadamu vimekitwa katika kazi ya Mungu, na usimamizi wa Mungu unadhihirika tu kupitia vitendo na ushirikiano wa mwanadamu. Mwanadamu ni mfano wa kazi ya Mungu, na mlengwa wa kazi ya usimamizi mzima wa Mungu, na pia mazao ya kazi ya usimamizi wote wa Mungu. Iwapo Mungu angefanya kazi peke yake bila ushirika wa mwanadamu, basi pasingekuwepo na kitu cha kudhihirisha kazi Yake nzima na kwa hali hiyo kusingekuwa na umuhimu hata kidogo wa usimamizi wa Mungu. Kando na kazi ya Mungu, ni kwa Mungu kuchagua vyombo vinavyofaa ili kuonyesha kazi Yake tu, na kuthibitisha kudura na busara zake, ndiyo inawezekana kufikia dhumuni la usimamizi wa Mungu na kufikia dhumuni la kutumia kazi hii yote ili kumshinda kabisa Shetani. Na kwa hivyo mwanadamu ni sehemu muhimu katika kazi ya usimamizi ya Mungu, na mwanadamu ndiye pekee anayeweza kuifanya kazi ya usimamizi ya Mungu ize

matunda na kufikia lengo Lake kuu; mbali na mwanadamu, hakuna kiumbe kingine chenye uhai kinachoweza kuchukua nafasi hiyo. Ikiwa mwanadamu atakuwa dhihirisho kamili la kazi ya usimamizi, basi uasi wa wanadamu wenye maovu lazima utokomezwe. Hii inahitaji kuwa mwanadamu apewe utendaji ufaao kwa kila muktadha, na kwamba Mungu afanye kazi inayotangamana miongoni mwa wanadamu. Ni kwa njia hii tu ndipo kutakuwa na kundi la watu waliokubaliwa ambao ni dhihirisho la kazi ya usimamizi. Kazi ya Mungu miongoni mwa wanadamu haiwezi kuwa ushuhuda kwa Mungu Mwenyewe kupitia kazi ya Mungu peke yake; ushuhuda huo vilevile unahitaji wanadamu ambao wanafaa ili kazi yake iafikiwe. Mwanzo Mungu atawatayarisha watu hawa ambao kupitia kwao kazi Yake itadhihirika na ushuhuda Wake utachukuliwa miongoni mwa viumbe. Kwa hili, Mungu atakuwa ameafiki lengo la kazi Yake. Mungu hafanyi kazi peke Yake kumshinda Shetani kwa sababu Mungu hawezi kujishuhudia Mwenyewe moja kwa moja miongoni mwa viumbe wote. Angefanya hivyo, ingekuwa vigumu kumshawishi mwanadamu, kwa hivyo Mungu lazima Afanye kazi kwa mwanadamu ili kumshinda na ndipo Atakapoweza kupata ushuhuda miongoni mwa viumbe vyote. Mungu angefanya kazi peke Yake bila kushirikiana na mwanadamu, au kama mwanadamu asingetakiwa kushirikiana, basi mwanadamu asingeitambua tabia ya Mungu na daima asingefahamu nia ya Mungu; na kwa hali hii haiwezi kuitwa usimamizi wa Mungu. Mwanadamu mwenyewe angejizatiti, na kutafuta, na kufanya bidii, bila kuifahamu kazi ya Mungu, basi mwanadamu angekuwa anafanya mizaha. Bila kazi ya Roho Mtakatifu, akifanyacho mwanadamu ni cha Shetani, ni muasi na mtenda maovu; Shetani anadhihirika katika yote yafanywayo na mwanadamu mwenye maovu na hamna kinachoafikiana na Mungu, na yote ni dalili ya Shetani. Hakuna kati ya vilivyozungumziwa kisichokuwa na maono na vitendo. Katika msingi wa maono, mwanadamu hupata vitendo na njia ya utiifu, ili kwamba aweze kuweka kando mawazo yake ili apate vile ambavyo hajawahi kuwa navyo hapo awali. Mungu huhitaji mwanadamu ashirikiane naye, kwamba mwanadamu asikilize matakwa Yake, na mwanadamu ashikilie kazi ifanywayo na Mungu Mwenyewe na kuupitia uwezo mkubwa wa Mungu na kuifahamu tabia ya Mungu. Kwa kifupi, haya ndiyo usimamizi wa Mungu. Ushirika wa Mungu na mwanadamu ndio usimamizi, na ni usimamizi mkuu zaidi.

Kile kinachohusisha maono kimsingi hurejelea kazi ya Mungu Mwenyewe, na kile kinachohusisha vitendo ni sharti kifanywe na mwanadamu, na hakina uhusiano na Mungu. Kazi ya Mungu hukamilishwa na Mungu Mwenyewe, na vitendo vya mwanadamu hufikiwa na mwanadamu mwenyewe. Kile ambacho ni sharti kifanywe na Mungu Mwenyewe hakihitajiki kufanywa na mwanadamu, na kile kitendwacho na mwanadamu hakihusiani na Mungu. Kazi ya Mungu ni huduma Yake Mwenyewe na haina uhusiano na mwanadamu. Hii kazi haihitaji kufanywa na mwanadamu, na hata zaidi, mwanadamu hatakuwa na uwezo wa kufanya kazi

ambayo ni ya kufanywa na Mungu. Kile ambacho kinafaa kutendwa na mwanadamu ni sharti kitimizwe na mwanadamu, iwe ni kujitoa kafara au kuwasilishwa kwake kwa Shetani ili kushuhudia—haya ni lazima yatimizwe na mwanadamu. Mungu Mwenyewe anatimiza kazi Yake yote, na kile ambacho ni wajibu wa mwanadamu, mwanadamu hufunuliwa na kazi iliyobaki huachiwa mwanadamu. Mungu hafanyi kazi ya ziada. Anafanya ile kazi iliyo katika huduma Yake na kumuonyesha mwanadamu na kumfunulia njia tu bali hampambanulii njia; hili lazima lieleweke kwa mwanadamu. Kuweka ukweli katika vitendo kunamaanisha kuweka neno la Mungu katika vitendo, na haya yote ni wajibu wa mwanadamu, ni kile kinachofaa kufanywa na mwanadamu, na wala halihusiani na Mungu. Iwapo mwanadamu atataka Mungu apitie masaiibu na utakaso katika ukweli sawa na mwanadamu, basi mwanadamu atakuwa hatii. Kazi ya Mungu ni kuendeleza huduma Yake, na wajibu wa mwanadamu ni kutii uongozi wote wa Mungu, bila pingamizi yoyote. Kinachotakiwa kufikiwa na mwanadamu anawajibika kutimiza, bila kujali ni namna gani Mungu hufanya kazi au kuishi. Ni Mungu Mwenyewe tu ndiye anayeweza kumwekea mwanadamu matakwa, ambayo ni kusema, ni Mungu Mwenyewe tu ndiye anayestahili kumwekea mwanadamu matakwa. Mwanadamu hastahili kuwa na jingine, hastahili kufanya chochote ila tu kutii kikamilifu na kutenda; hii ndiyo busara ambayo mwanadamu anapaswa kuwa nayo. Punde kazi ifaayo kufanywa na Mungu Mwenyewe itakapokamilika, mwanadamu anatakiwa kuipitia, hatua kwa hatua. Iwapo mwishowe, baada ya usimamizi wote wa Mungu kukamilika, mwanadamu atakuwa hajafanya anachotakiwa na Mungu kufanya, basi mwanadamu anafaa aadhibiwe. Ikiwa mwanadamu hatimizi matakwa ya Mungu, basi hili ni kwa sababu ya uasi wa mwanadamu; haimaanishi kuwa Mungu hajakuwa makini vya kutosha katika kazi Yake. Wale wote wasioweka neno la Mungu katika vitendo, ambao hawatimizi matakwa ya Mungu na wale wote wasiokuwa na uaminifu na kutimiza wajibu wao—wataadhibiwa wote. Leo hii mnachohitajika kufikia si madai ya ziada, ila ni wajibu wa mwanadamu, na kile kinachofaa kufanywa na kila mtu. Kama hamuwezi hata kufanya wajibu wenu, au kuufanya vizuri, hamuoni mnajiletea masaiibu nyinyi wenyewe? Hamwuoni mnajitakia kifo? Mtatarajiaje maisha ya baadaye na matarajio? Kazi ya Mungu ni kwa ajili ya wanadamu, na ushirika wa mwanadamu ni kwa minajili ya usimamizi wa Mungu. Baada ya Mungu kufanya yale yote Anayopaswa kufanya, mwanadamu anapaswa kufanya vitendo bila kukoma, na kushirikiana na Mungu. Mwanadamu hapaswi kulegeza kamba katika kazi ya Mungu, lazima aonyeshe uaminifu na asijitie katika mawazo mengi au kukaa akisubiri kifo bila kufanya kitu. Mungu Mwenyewe anaweza kujitolea kwa mwanadamu, basi ni kwa nini mwanadamu asiweze kuwa mwaminifu kwa Mungu? Mawazo na moyo wa Mungu vipo kwa mwanadamu, basi ni kwa nini mwanadamu asijitolee katika ushirika? Mungu huwafanyia wanadamu kazi, basi ni kwa nini mwanadamu asifanye wajibu wake kwa minajili ya usimamizi wa Mungu? Kazi ya Mungu imefika umbali huu, bado mnaona ila hutendi, mnasikia ila hamsogei. Je, si watu kama hawa

wanafaa kuangamizwa kabisa? Tayari Mungu amejitolea kikamilifu kwa ajili ya mwanadamu, basi ni kwa nini siku hizi mwanadamu hafanyi wajibu wake kwa dhati? Kwa Mungu, kazi Yake ni ya kipaumbele Kwake, na kazi ya usimamizi Wake ni ya umuhimu wa hali ya juu. Kwa mwanadamu, kuweka maneno ya Mungu katika vitendo na kutimiza mahitaji ya Mungu ndiyo kipaumbele kwake. Ni lazima nyote myafahamu haya. Maneno mliyoambiwa yamefika kiini halisi cha nafsi yenu, na kazi ya Mungu imefika katika maeneo ambayo hayakuwa yamefikiwa awali. Watu wengi bado hawafahamu ukweli na uongo wa njia hii; bado wanasubiri na kutazama na hawafanyi wajibu wao. Badala yake huchunguza kila neno na tendo la Mungu, wanalenga juu ya Anachokula na Anachokivaa na mawazo yao huwa hata ya kuhuzunisha zaidi. Si watu wa aina hii wanafanya msukosuko bure? Hawa wanawezaje kuwa watu wamtafutao Mungu? Na wanawezaje kuwa watu wenye dhamira ya kunyenyekea kwa Mungu? Wanasahau uaminifu na wajibu wao na badala yake kujishughulisha na mahali alipo Mungu. Wanaghadhabisha! Ikiwa mwanadamu amefahamu yale yote anayopaswa kufahamu na kuweka katika vitendo yale yote anayopaswa, basi Mungu atampa mwanadamu baraka Zake, kwa sababu kile ambacho Yeye huhitaji kutoka kwa mwanadamu ni wajibu wa mwanadamu, na kile ambacho mwanadamu anastahili kufanya. Ikiwa mwanadamu hawezi kufahamu yale yote anayopaswa kufahamu na hawezi kutia katika vitendo yale anayopaswa kuweka katika vitendo, basi mwanadamu ataadhibiwa. Wasioshirikiana na Mungu wana uhasama Naye, wasioikubali kazi mpya wanaipinga, hata kama watu kama hao hawafanyi chochote ambacho ni cha pingamizi dhahiri. Wale wote wasioweka ukweli unaohitajika na Mungu katika vitendo ni watu wanaopinga kwa makusudi na ni waasi wa maneno ya Mungu hata kama watu kama hawa hutilia maanani maalum kwa kazi ya Roho Mtakatifu. Watu wasiotii maneno ya Mungu na kumnyenyekea Mungu ni waasi, na wapinzani wa Mungu. Watu wasiofanya wajibu wao ni wale wasioshirikiana na Mungu, na watu wasioshirikiana na Mungu ni wale wasioikubali kazi ya Roho Mtakatifu.

Wakati kazi ya Mungu inafikia hatua fulani, na usimamizi Wake kufikia hatua fulani, wale wanaoutafuta moyo Wake wote huwa na uwezo wa kutimiza matakwa yake. Mungu humwekea mwanadamu matakwa kulingana na viwango Vyake mwenyewe, na kulingana na kile ambacho mwanadamu anaweza kufanikisha. Akiwa anazungumzia usimamizi Wake, Yeye humwonyesha njia mwanadamu, na kumpa mwanadamu namna ya kudumu. Usimamizi wa Mungu na vitendo vya mwanadamu vipo katika hatua sawia kikazi, na yote yanafanyika kwa wakati mmoja. Mazungumzo kuhusu usimamizi wa Mungu yanagusia mabadiliko katika tabia ya mwanadamu, na yanazungumzia kuhusu yale yafaayo kufanywa na mwanadamu, na mabadiliko katika tabia ya mwanadamu, hugusia kazi ya Mungu; hakuna wakati ambao haya mawili yanaweza kutenganishwa. Vitendo vya mwanadamu vinabadilika, hatua kwa hatua. Hii ni kwa sababu matakwa ya Mungu kwa mwanadamu yanabadilika na vilevile kwa sababu kazi ya Mungu

hubadilika na kusonga mbele kila wakati. Iwapo vitendo vya mwanadamu vitasalia ndani ya mafundisho, hii inathibitisha kwamba amepungukiwa na kazi na mwongozo wa Mungu; ikiwa vitendo vya mwanadamu havitabadilika kamwe au kuwa na kina zaidi, basi hili ni thibitisho kwamba vitendo vya mwanadamu hutendeka kulingana na mapenzi ya mwanadamu, na si vitendo vya ukweli; ikiwa mwanadamu hana njia ya kufuata, basi tayari ameanguka mikononi mwa Shetani, na sasa amedhibitiwa na Shetani, ambayo inamaanisha kwamba amedhibitiwa na roho mchafu. Ikiwa vitendo vya mwanadamu haviendi ndani zaidi, basi kazi ya Mungu haitakua, na kama hakuna mabadiliko katika kazi ya Mungu, basi kuingia kwa mwanadamu kutakwama; hili haliepukiki. Katika kazi nzima ya Mungu, mwanadamu angejifunga katika sheria za Yehova basi kazi ya Mungu isingendelee na zaidi ingekuwa vigumu kutamatisha enzi nzima. Iwapo mwanadamu angeshikilia msalaba daima na kuishi katika uvumilivu na unyenyekevu, basi kazi ya Mungu isingendelee. Miaka elfu sita ya usimamizi haiwezi kusitishwa miongoni mwa watu wanaoshikilia tu sheria au kushikilia msalaba na kuishi katika uvumilivu na unyenyekevu tu. Badala yake, kazi nzima ya usimamizi wa Mungu inahitimishwa miongoni mwa watu wa siku za mwisho wanaomfahamu Mungu na ambao wamekombolewa kutoka kwa Shetani na wamejinasua kabisa kutoka katika vishawishi vya Shetani. Huu ni mwelekeo wa kazi ya Mungu usioepukika. Kwa nini inasemekana kwamba vitendo vya walio katika makanisa ya kidini vimepitwa na wakati? Ni kwa kuwa wanayoyaweka katika vitendo ni tofauti na kazi ya leo. Katika Enzi ya Neema, walichotenda kilikuwa sahihi, ila kwa kuwa enzi yenyewe imepita na kazi ya Mungu kubadilika, vitendo vyao hatua kwa hatua vimepitwa na wakati. Vimeachwa nyuma na kazi mpya na mwangaza mpya. Ikiwa imesimama juu ya msingi wake asili, kazi ya Roho Mtakatifu imepiga hatua kadhaa kwa kina. Na bado watu hao wamebaki katika hatua ya asili ya kazi ya Mungu na bado wanapenyeza katikati ya vitendo na mwangaza wa zamani. Kazi ya Mungu yaweza kubadilika pakubwa kwa miaka mitatu au mitano, hivyo si mabadiliko hata makubwa zaidi yaweza kuja kwa kipindi cha miaka zaidi ya 2000? Ikiwa mwanadamu hana vitendo vipya ama mwangaza mpya, inamaanisha hajaenda sawia na kazi ya Roho Mtakatifu. Hili ni anguko la mwanadamu; uwepo wa kazi mpya ya Mungu hauwezi kukanwa kwa sababu, leo hii, wale waliokuwa na kazi ya Roho Mtakatifu hapo awali bado wanashikilia vitendo vilivyopitwa na wakati. Kazi ya Roho Mtakatifu daima inasonga mbele, na wote walio katika mkondo wa Roho Mtakatifu wanafaa waendeleo mbele na kubadilika, hatua kwa hatua. Hawapaswi kukwama katika hatua moja. Ni wale tu wasioifahamu kazi ya Roho Mtakatifu ndio wanaweza kubaki katika hatua ya kazi ya Mungu ya awali na wasikubali kazi mpya ya Roho Mtakatifu. Ni wale tu walio waasi ndio watakosa uwezo wa kuipokea kazi ya Roho Mtakatifu. Ikiwa vitendo vya mwanadamu haviendani na mwendo wa kazi mpya ya Roho Mtakatifu, basi vitendo vya mwanadamu hakika vimetengana na kazi ya leo na kwa hakika havilingani na kazi ya leo. Watu waliopitwa na wakati kama hawa hawawezi kutimiza mapenzi ya Mungu, sembuse

kuwa wale watu watakaomshuhudia Mungu hatimaye. Aidha, kazi nzima ya usimamizi haiwezi kutimilika miongoni mwa kundi la watu kama hao. Kwa wale walioshikilia sheria za Yehova kipindi fulani, na wale walioumia wakati fulani chini ya msalaba, ikiwa hawawezi kukubali hatua ya kazi ya siku za mwisho, basi yale yote waliyofanya ni bure na yasiyofaa. Dhihirisho la wazi zaidi wa kazi ya Roho Mtakatifu ni kwa kuyakumbatia ya sasa, sio kushikilia ya zamani. Wale ambao hawajiendelezi na kazi ya leo, na wale ambao wametengwa na utendaji wa leo, ni wale wanaopinga na hawaikubali kazi ya Roho Mtakatifu. Watu kama hao wanaipinga kazi ya Mungu ya sasa. Ijapokuwa wanashikilia nuru ya zamani, hili halimaanishi kwamba inaweza kukanwa kwamba hawajui kazi ya Roho Mtakatifu. Kwa nini kumekuwepo na mjadala huu wote kuhusu mabadiliko katika vitendo vya mwanadamu, kuhusu tofauti za utendaji kati ya zamani na sasa, kuhusu jinsi utendaji ulivyokuwa katika enzi za awali na jinsi ulivyo sasa? Migawanyiko kama hiyo katika vitendo vya mwanadamu hujadiliwa kwa sababu kazi ya Roho Mtakatifu daima inasonga mbele na kwa hivyo vitendo vya mwanadamu vinapaswa kubadilika daima. Ikiwa mwanadamu atasalia amekwama katika hatua moja tu, basi hili linaonyesha kuwa haendi sawia na kazi mpya na mwangaza mpya wa Mungu; haimaanishi kuwa mpango wa usimamizi wa Mungu haujabadilika. Walio nje ya mkondo wa Roho Mtakatifu daima hudhani wako sahihi, lakini kwa hakika, kazi ya Mungu ndani yao ilisita zamani na kazi ya Roho Mtakatifu haimo ndani yao. Kazi ya Mungu imeshahamishiwa kwa kundi jingine la watu, kundi ambalo kwalo Anapania kukamilishia kazi Yake mpya. Kwani walio katika dini hawawezi kuikubali kazi mpya ya Mungu, na kushikilia tu kazi kongwe za zamani, hivyo Mungu amewaacha watu hawa na anafanya kazi Yake mpya kwa watu wanaoikubali kazi hii mpya. Hawa ni watu wanaoshiriki katika kazi Yake mpya, na usimamizi Wake utatimilika kwa njia hii tu. Usimamizi wa Mungu daima unasonga mbele na vitendo vya mwanadamu daima vinapanda juu. Mungu daima anafanya kazi na mwanadamu mara zote ni mhitaji ili kwamba wote wanafikia upeo wao, Mungu na mwanadamu wamo katika muungano kikamilifu. Haya ni maonyesho ya kutimilika kwa kazi ya Mungu, na ndiyo matokeo ya mwisho ya kazi nzima ya usimamizi.

Katika kila hatua ya kazi ya Mungu yapo pia matakwa sawia kwa mwanadamu. Wale wote walio katika mkondo wa Roho Mtakatifu wanamilikiwa na uwepo na nidhamu ya Roho Mtakatifu na wasiokuwemo katika mkondo wa Roho Mtakatifu wako chini ya utawala wa Shetani na hawana kazi yoyote ya Roho Mtakatifu. Walio katika mkondo wa Roho Mtakatifu ni wale wanaoikubali kazi mpya ya Mungu, wanaoshiriki katika kazi mpya ya Mungu. Iwapo walio ndani ya mkondo huu hawana uwezo wa kushirikiana, na hawawezi kuweka ukweli unaotakiwa na Mungu katika vitendo wakati huu, basi watafundishwa nidhamu, na hali ikiwa mbaya zaidi kuachwa na Roho Mtakatifu. Wale ambao wanakubali kazi mpya ya Roho Mtakatifu, wataishi katika mkondo wa Roho Mtakatifu, wapokee utunzaji na ulinzi wa Roho Mtakatifu. Wale ambao

wako tayari kuweka ukweli katika vitendo wanapewa nuru na Roho Mtakatifu na wale wasiotaka kuweka ukweli katika vitendo wanafundishwa nidhamu na Roho Mtakatifu na huenda hata wakaadhibiwa. Bila kujali wao ni aina gani ya watu, ilimradi tu wamo katika mkondo wa Roho Mtakatifu, Mungu atawawajibikia wote wanaoikubali kazi Yake mpya kwa minajili ya jina Lake. Wale wanaolitukuza jina Lake na wako radhi kuweka maneno Yake katika vitendo watapokea baraka Zake; wale wasiomtii na wasioyaweke maneno Yake katika vitendo watapokea adhabu Yake. Watu walio katika mkondo wa Roho Mtakatifu ni wale wanaoikubali kazi mpya, na kwa sababu wameikubali kazi mpya, wanafaa kuwa na ushirika wa kufaa na Mungu na hawafai kuwa kama waasi wasiofanya wajibu wao. Hili ndilo sharti la pekee la Mungu kwa mwanadamu. Sio hivyo kwa watu wasioikubali kazi mpya: Wako nje ya mkondo wa Roho Mtakatifu, na nidhamu na lawama ya Roho Mtakatifu hayatumiki kwao. Kila siku hawa watu wanaishi ndani ya mwili, wanaishi ndani ya akili zao, na yote wayafanyayo ni kulingana na mafundisho ya kidini yaliyozalishwa na uchanganuzi pamoja na utafiti wa bongo zao. Si matakwa ya kazi mpya ya Roho Mtakatifu sembuse ushirika na Mungu. Wale wasioikubali kazi mpya ya Mungu hawana uwepo wa Mungu na, zaidi, wanakosa baraka na ulinzi wa Mungu. Maneno na matendo yao mengi yanashikilia matakwa ya zamani ya kazi ya Roho Mtakatifu; ni mafundisho ya kidini, si ukweli. Mafundisho na taratibu kama hizo ni thibitisho la kutosha kuwa kukutana pamoja kwa watu hawa si lingine ila dini; si watu walioteuliwa au vyombo vya kazi ya Mungu. Mkutano wa wale wote walio miongoni mwao unaweza tu kuitwa mkutano mkubwa wa watu wa dini, na bali hauwezi kuitwa kanisa. Huu ni ukweli usioweza kubadilishwa. Hawana kazi mpya ya Roho Mtakatifu; wakifanyacho kinaonekana chenye kunuka dini, wanachoishi kwa kudhihirisha katika maisha yao kinaonekana kimejaa dini; hawana uwepo na kazi ya Roho Mtakatifu, sembuse kustahiki kupokea nidhamu au nuru ya Roho Mtakatifu. Watu hawa wote ni miili isiyo na uhai, na funza wasio na mambo ya kiroho. Hawana ufahamu wa uasi na pingamizi wa mwanadamu, hawana ufahamu wa uovu wote wa mwanadamu, sembuse kujua kazi yote ya Mungu na mapenzi ya sasa ya Mungu. Wote ni watu wapumbavu, waovu, ni watu duni wasiostahili kuitwa waumini! Hakuna wafanyacho kinachohusiana na usimamizi wa Mungu, sembuse kuweza kuidhoofisha mipango ya Mungu. Maneno na matendo yao yanaudhi sana, yanasikitisha mno, na hayafai kutajwa kabisa. Hakuna chochote wakifanyacho walio nje ya mkondo wa Roho Mtakatifu kinahusiana na kazi mpya ya Roho Mtakatifu hata kidogo. Kwa sababu hii, haijalishi wanafanya nini, hawana nidhamu ya Roho Mtakatifu na zaidi, hawana nuru ya Roho Mtakatifu. Kwani wao ni watu wasiopenda ukweli, na wamechukiwa na kukataliwa na Roho Mtakatifu. Wanaitwa watenda maovu kwani wanatembea katika mwili, na kufanya chochote kiwafurahishacho kwa kisingizio cha bango la Mungu. Mungu anapofanya kazi, wao wanakuwa maadui Kwake kwa makusudi, na kumkimbia Yeye. Kutoweza kushirikiana kwa mwanadamu na Mungu ni uasi wa hali ya juu, kwa hivyo wale watu wanaokimbia kinyume na Mungu makusudi si watapokea

hakika malipo yao ya haki? Uovu wa hawa watu unapotajwa, baadhi ya watu wanakuwa na hamu ya kuwalaani, huku Mungu akiwapuuza. Kwa mwanadamu, inaonekana kana kwamba matendo ya watu hawa yanahusisha jina la Mungu, ila kwa hakika, kwa Mungu, hayana uhusiano wowote na jina Lake au ushuhuda Kwake. Bila kujali wanachokifanya hawa watu, hakihusiani na Mungu: hakihusiani na kazi Yake na jina Lake leo. Hawa watu hujiabisha wenyewe na kumdhihirisha Shetani; ni watenda maovu wanaohodhi wakisubiri siku ya ghadhabu. Sasa, bila kujali matendo yao ni yapi, na alimradi tu hawazuii usimamizi wa Mungu na hawafanyi chochote kuhusiana na kazi mpya ya Mungu, watu kama hao hawatapata adhabu inayolingana na matendo yao, kwa kuwa siku ya ghadhabu bado haijatimia. Yapo mengi ambayo watu wanaamini kuwa Mungu angekuwa ameyashughulikia tayari, na wanafikiri kuwa wale watenda maovu wanastahili kuadhibiwa haraka iwezekanavyo. Lakini kwa sababu kazi ya usimamizi wa Mungu bado haijafikia kikomo, na siku ya ghadhabu haijatimia bado, wadhalimu bado wanaendelea kutenda matendo yao maovu. Watu wengine husema, “Walio ndani ya dini hawana uwepo au kazi ya Roho Mtakatifu, na wanaliletea jina la Mungu aibu; basi ni kwa nini Mungu asiwaangamize, badala ya kuendelea kustahimili tabia yao isiyo na nidhamu?” Watu hawa ambao ni dhihirisho la Shetani na ambao wanaonyesha mwili, ni watu wapumbavu, wa hali duni, ni watu wa upuuzi. Hawataiona kufika kwa ghadhabu ya Mungu kabla ya wao kuelewa jinsi Mungu anavyofanya kazi Yake miongoni mwa wanadamu, na wakishashindwa kabisa, hao watenda maovu wote watapata adhabu yao, na hakuna hata mmoja kati yao atakayeweza kuiepuka siku ya ghadhabu. Sasa si wakati wa adhabu ya mwanadamu, ila ni wakati wa kutekeleza kazi ya ushindi, isipokuwa kama kuna wale wanaoiharibu kazi ya usimamizi wa Mungu, ambao wataadhibiwa kulingana na uzito wa matendo yao kama ni hivyo. Katika kipindi cha usimamizi wa Mungu wa wanadamu, wote walio ndani ya mkondo wa Roho Mtakatifu huwa na uhusiano na Mungu. Wale wanaochukiwa na kukataliwa na Roho Mtakatifu huishi katika ushawishi wa Shetani na kile wawekacho katika vitendo hakina uhusiano na Mungu. Wanaoikubali kazi mpya ya Mungu tu, na wanaoshirikiana na Mungu ndio wana uhusiano na Mungu, kwani kazi ya Mungu inakusudiwa tu kwa watu wanaoikubali wala si watu wote, haijalishi kama wanaikubali au la. Kazi inayofanywa na Mungu daima ina kusudi, na haifanywi kwa ghafla. Walio na uhusiano na Shetani hawafai kuwa na ushuhuda kwa Mungu, sembuse kufaa kushirikiana na Mungu.

Kila hatua ya kazi ya Roho Mtakatifu inahitaji kwa sawia ushuhuda kutoka kwa mwanadamu. Kila hatua ya kazi ni vita kati ya Mungu na Shetani, na mlengwa katika vita hivi ni Shetani, huku atakayekamilishwa na kazi hii ni mwanadamu. Kazi ya Mungu kuweza kuzaa au kutozaa matunda kunategemea jinsi ushuhuda wa mwanadamu kwa Mungu ulivyo. Huu ushuhuda ndio Mungu anaohitaji kutoka kwa wale wanaomfuata; ni ushuhuda unaofanywa

mbele ya Shetani, na pia unaothibitisha athari za kazi Yake. Usimamizi mzima wa Mungu umegawika katika hatua tatu, na katika kila hatua, mahitaji yanayofaa yanatakiwa kutoka kwa mwanadamu. Aidha, kadri enzi zinavyopita na kuendelea, mahitaji ya Mungu kwa wanadamu wote huwa ya juu hata zaidi. Kwa hiyo, hatua kwa hatua, kazi hii ya usimamizi wa Mungu hufikia kilele chake, hadi mwanadamu aamini ukweli wa “kuonekana kwa Neno katika mwili,” na kwa njia hii mahitaji ya mwanadamu huwa ya juu hata zaidi, na mahitaji ya mwanadamu kutoa ushuhuda huwa ya juu hata zaidi. Kadiri mwanadamu alivyo na uwezo wa kushirikiana na Mungu kwa kweli, ndivyo anavyozidi kumtukuza Mungu. Ushirikiano wa mwanadamu ndio ushuhuda anaohitajika kuwa nao, na ushuhuda alio nao ndio matendo ya mwanadamu. Na kwa hivyo, kazi ya Mungu iweze au isiweze kuwa na matokeo yanayohitajika, na paweze ama pasiweze kuwa na ushuhuda wa kweli, ni mambo ambayo yameunganishwa yasiyochanganulika na ushirikiano na ushuhuda wa mwanadamu. Wakati kazi itakapokwisha, yaani, wakati usimamizi wote wa Mungu utakapofikia kikomo chake, mwanadamu atahitajika kuwa na ushuhuda wa hali ya juu, na wakati kazi ya Mungu itakapofika mwisho wake, matendo na kuingia kwa mwanadamu vitafikia upeo wake. Wakati wa kale, mwanadamu alihitajika kutii sheria na amri, na alihitajika kuwa mwenye subira na mnyenyekevu. Leo, mwanadamu anahitajika kutii mipango yote ya Mungu na awe na upendo mkuu wa Mungu, na hatimaye bado anahitajika kumpenda Mungu katika taabu. Hatua hizi tatu ndizo Mungu anazozitazamia kutoka kwa mwanadamu, hatua kwa hatua, katika usimamizi Wake wote. Kila hatua ya kazi ya Mungu huzidisha kina kuliko iliyopita, na katika kila hatua, mahitaji kwa mwanadamu ni makubwa kuliko yaliyopita, na kwa njia hii, usimamizi mzima wa Mungu huonekana. Ni hasa kwa sababu mahitaji ya mwanadamu kila mara huwa ya juu kiasi kwamba tabia yake kila mara inafikia viwango anavyovihitaji Mungu, na ni hapo tu ambapo wanadamu wote wanaanza kujiondoa polepole kutoka kwa ushawishi wa Shetani hadi, ambapo kazi ya Mungu itafikia kikomo kabisa, ndio wanadamu wote watakuwa wameokolewa kutoka kwa ushawishi wa Shetani. Wakati huo utakapowadia, kazi ya Mungu itakuwa imefika mwisho wake, na ushirikiano wa mwanadamu na Mungu ili kufikia mabadiliko katika tabia yake hautakuwepo tena, na wanadamu wote wataishi katika nuru ya Mungu, na kuanzia hapo kuendelea, hapatakuwa na uasi au upinzani wowote kwa Mungu. Pia Mungu hatamwekea mwanadamu matakwa, na patakuwepo na ushirikiano wenye upatanifu zaidi kati ya mwanadamu na Mungu, ambao utakuwa maisha ya mwanadamu na Mungu pamoja, maisha ambayo yatafuatia baada ya usimamizi wa Mungu kukamilishwa kabisa, na baada ya mwanadamu kuokolewa kikamilifu kutoka katika mafumbato ya Shetani. Wale ambao hawawezi kutafuata kwa ukaribu nyayo za Mungu hawana uwezo wa kufikia maisha kama hayo. Watakuwa wamejishusha ndani ya giza, ambapo watalia na kusaga meno; hao ndio watu wanaoamini katika Mungu lakini hawamfuati Yeye, wanaoamini katika Mungu lakini hawatii kazi Yake yote. Kwa kuwa mwanadamu anamwamini Mungu, ni sharti afuate kwa

ukaribu nyayo Zake, hatua kwa hatua; anapaswa “kumfuata Mwanakondoo popote Aendapo.” Hawa tu ndio watu wanaotafuta njia ya kweli, na wao tu ndio wanaoifahamu kazi ya Roho Mtakatifu. Watu wanaofuata tu kanuni na mafundisho ya dini kiutumwa ni wale ambao wameondolewa na kazi ya Roho Mtakatifu. Katika kila kipindi cha wakati, Mungu ataanza kazi mpya, na katika kila kipindi, patakuwepo na mwanzo mpya kwa mwanadamu. Laiti mwanadamu ashikilie tu ukweli kwamba “Yehova ni Mungu” na “Yesu ni Kristo,” ambao ni ukweli unaozingatiwa katika enzi moja tu, basi mwanadamu hatawahi kwenda sambamba na kazi ya Roho Mtakatifu, na daima hataweza kupokea kazi ya Roho Mtakatifu. Bila kujali jinsi Mungu anavyofanya, mwanadamu anafaa kufuata bila shaka lolote, na afuate kwa ukaribu. Kwa jinsi hii basi itakuwaje mwanadamu aondolewe na Roho Mtakatifu? Bila kujali kile anachofanya Mungu, kama mwanadamu ana uhakika ni kazi ya Roho Mtakatifu, na kushirikiana katika kazi ya Roho Mtakatifu bila mashaka yoyote, na kujaribu kufikia mahitaji ya Mungu, basi ataadhibiwaje? Kazi ya Mungu kamwe haijasimama, hatua Zake hazijakwama na kabla kukamilisha kazi Yake ya usimamizi, siku zote Mungu amekuwa mwenye kazi nyingi, na kamwe hajasimama. Lakini mwanadamu ni tofauti: Kutokana na kupata kiwango cha chini cha nguvu za Roho Mtakatifu, yeye huchukulia kwamba hakuna chochote kitakachobadilika; baada ya kupata ufahamu kidogo, hajipi msukumo wa kufuata nyayo za kazi mpya ya Mungu; licha ya kwamba ameona kiasi kazi ya Mungu, yeye anamchukulia Mungu kama kifaa, aina fulani ya umbo la sanamu ya mti, na anaamini kwamba Mungu atasalia kuwa hivyo daima kwani hali imekuwa hii tangu hapo awali na hata katika siku zijazo; akiwa amepata ufahamu wa kijuujuu, mwanadamu ni mwenye kiburi hivi kwamba hujisahau na kuanza kutangaza kwa fujo tabia ya Mungu na hali ya Mungu ambayo haipo; na akiwa na uhakika juu ya hatua moja ya Roho Mtakatifu, pasi kujali ni mtu wa aina gani ambaye anatangaza kazi mpya ya Mungu, mwanadamu huwa haikubali. Hawa ni watu ambao hawawezi kuikubali kazi mpya ya Roho Mtakatifu; ni watu wenye kushikilia ukale sana, na hawawezi kukubali mambo mapya. Watu kama hawa ni watu wanaomwamini Mungu lakini wakati uo huo wanamkataa Mungu. Mwanadamu anaamini kwamba wana wa Israeli walikosea “tu kumuamini Yehova na kukosa kumuamini Yesu,” huku watu wengi wakiiga jukumu ambapo “humwamini Yehova tu na kumkataa Yesu” na “kusubiri kwa hamu kurejea kwa Masihi lakini wanamkataa Masihi ambaye ni Yesu”. Ndiyo maana, basi, watu wengi bado wanaishi chini ya mamlaka ya Shetani baada ya kukubali hatua moja tu ya Roho Mtakatifu na bado hawapokei baraka za Mungu. Je, si hii ni kutokana na uasi wa mwanadamu? Wakristo ulimwenguni kote ambao hawajazingatia kazi mpya ya sasa wote wameshikilia imani kwamba wao ni wenye bahati na kwamba Mungu atawatimizia kila mojawapo ya malengo yao. Lakini hawawezi kueleza mbona Mungu atawapeleka katika mbingu ya tatu na wala hawafahamu jinsi Yesu atakavyokuja juu ya wingu jeupe na kuwachukua, wala kusema kwa uhakika kamili kama kweli Yesu atawasili akiwa juu ya wingu jeupe siku ambayo wanaiwaza. Wote wana wasiwasi, na kukanganywa; wao

wenyewe hata hawafahamu kama Mungu atachukua kila mmoja wao, watu wachache sana, wanaotoka katika madhehebu yote. Kazi ambayo Mungu anafanya kwa sasa, enzi ya sasa, mapenzi ya Mungu—ni vitu ambavyo watu hawavifahamu, na hawana cha kufanya bali kusubiri na kuhesabu siku katika vidole vyao. Ni wale tu wanaofuata nyayo za Mwanakondoo hadi mwisho kabisa ndio wanaoweza kufaidi baraka za mwisho, huku wale “watu werevu,” ambao hawawezi kumfuata hadi mwisho ilhali wanaamini wamepata yote, ndio wasiokuwa na uwezo wa kushuhudia kuonekana kwa Mungu. Wote huamini wao ndio werevu zaidi duniani, na wanasitisha maendeleo ya kazi ya Mungu bila sababu yoyote kabisa, na huonekana kuamini pasi na shaka kwamba Mungu atawachukua mbinguni, wao “wenye uaminifu wa juu zaidi kwa Mungu, humfuata Mungu, na hutii neno la Mungu”. Hata ingawa wana “uaminifu wa hali ya juu” kwa maneno yaliyozungumzwa na Mungu; maneno yao na matendo yao bado hukera kwa sababu wao huipinga kazi ya Roho Mtakatifu, na kufanya uongo na uovu. Wale wasiofuata hadi mwisho kabisa, ambao hawazingatii kazi ya Roho Mtakatifu, na ambao wanashikilia kazi ya zamani hawajakosa tu kupata uaminifu kwa Mungu, bali kwa kinyume, wamekuwa wale wanaompinga Mungu, wamekuwa wale ambao wamekanwa na enzi mpya, na watakaoadhibiwa. Kuna wa kuhurumiwa zaidi kuliko wao? Wengi hata wanaamini kuwa wale wanaokana sheria ya zamani na kukubali kazi mpya hawana dhamiri. Watu hawa, ambao huongea tu kuhusu “dhamiri,” na hawajui kazi ya Roho Mtakatifu, hatimaye watapata kuwa matarajio yao yamekatizwa na dhamiri yao yenyewe. Kazi ya Mungu haizingatii mafundisho, na ingawa ni kazi Yake Mwenyewe, bado Mungu haishikili. Kile kinachopaswa kukataliwa kinakataliwa, kile kinachopaswa kuondolewa kinaondolewa. Lakini mwanadamu anajiweka kwenye uadui wa Mungu kwa kushikilia sehemu moja ndogo ya kazi ya usimamizi wa Mungu. Si huu ndio upuuzi wa mwanadamu? Si huu ndio ujinga wa mwanadamu? Kadri watu wanakuwa waoga na wenye tahadhari sana kwa sababu wanachelea kutopata baraka za Mungu, ndivyo wanavyopungukiwa zaidi na uwezo wa kupata baraka zaidi, na wa kupata ile baraka ya mwisho. Watu wale wanaoshikilia kiutumwa sheria huwa wanadhihirisha uaminifu wa hali ya juu kwa sheria, na kadri wanavyodhihirisha uaminifu jinsi hiyo kwa sheria, ndivyo wanavyokuwa waasi wanaompinga Mungu. Kwa kuwa sasa ni Enzi ya Ufalme na wala si Enzi ya Sheria, na kazi ya leo na kazi ya zamani haziwezi kulinganishwa, wala kazi ya zamani haiwezi kulinganishwa na kazi ya sasa. Kazi ya Mungu imebadilika, na vitendo vya mwanadamu pia vimebadilika; si kushikilia sheria au kuubeba msalaba. Basi, uaminifu wa watu kwa sheria na msalaba hautapata kibali cha Mungu.

Mwanadamu atakamilishwa kabisa katika Enzi ya Ufalme. Baada ya kazi ya ushindi, mwanadamu atapitishwa kwenye mambo magumu ya kusafishwa na taabu. Wale ambao wanaweza kushinda na kushuhudia katika taabu hii ndio hatimaye watakaofanywa wakamilifu;

wao ndio washindi. Katika taabu hii, mwanadamu anahitajika kukubali kusafishwa huku, na kusafishwa huku ndio tukio la mwisho la kazi ya Mungu. Itakuwa mara ya mwisho ambapo mwanadamu atasafishwa kabla ya hitimisho la kazi zote za usimamizi wa Mungu, na wale wote wanaomfuata Mungu lazima wakubali jaribio hili la mwisho, lazima wakubali kusafishwa huku kwa mwisho. Wale ambao wamekabiliwa na taabu ni wale wasiokuwa na kazi ya Roho Mtakatifu na uelekezi wa Mungu, lakini wale ambao wameshindwa kwa kweli na wanatafuta mapenzi ya Mungu kwa kweli hatimaye watasimama imara; ndio wale ambao wana ubinadamu, na wanaompenda Mungu kwa kweli. Bila kujali Mungu hufanya nini, hawa washindi hawatapungukiwa na maono, na bado watauweka ukweli katika matendo bila kufeli katika ushuhuda wao. Wao ndio watakaosimama mwishowe kutoka kwenye taabu kubwa. Hata ingawa wale wanaovua samaki katika maji yenye mawimbi mengi bado wanaweza kusaidiwa leo, hakuna yeyote atakayeepuka taabu, na hakuna atakayeepuka jaribio la mwisho. Kwa wale wanaoshinda, taabu ya aina hii ni usafisho mkubwa; lakini wale wanaovua katika maji yenye mawimbi, ni kazi ya kuondolewa kamili. Bila kujali jinsi wanavyojaribiwa, utii wa wale wenye Mungu ndani ya mioyo yao hubaki vile vile; lakini kwa wale wasiokuwa na Mungu ndani ya mioyo yao, wakati kazi ya Mungu hainufaishi miili yao, wanabadilisha mtazamo wao kwa Mungu, na hata kumkimbia Mungu. Hawa ndio wale hawatasimama imara mwishoni, wanaotafuta baraka za Mungu na hawana tamaa ya kujitolea wenyewe kwa Mungu na kujikabidhi wenyewe Kwake. Watu duni wa aina hii watafukuzwa wakati kazi ya Mungu itakapofikia kikomo, na wao hawafai kuonewa huruma yoyote. Wale wasiokuwa na ubinadamu, hawawezi kumpenda Mungu kwa kweli. Wakati mazingira ni mema na salama, au kama kuna faida inayoweza kupatwa, wao ni watiifu kabisa kwa Mungu, lakini wakati walilokuwa wanataka limepatikana au hatimaye kukataliwa, wanageuka mara moja. Hata kama ni kwa muda wa usiku mmoja tu, wao watatoka katika hali ya tabasamu, watu wenye “mioyo mikunjufu” hadi wenye sura mbovu na wauaji wakatili, ghafla wakiwatendea wafadhili wao wa jana kana kwamba ni adui wa milele, bila chanzo wala sababu. Ikiwa mapepo haya hayatarushwa nje, mapepo haya ambayo yanaweza kuua bila kusita, je, hayatakuwa hatari iliyofichika? Kazi ya kumwokoia mwanadamu haitimizwi kufuatia kazi ya kukamilisha ushindi. Ingawa kazi ya ushindi imefika kikomo, kazi ya kumtakasa mwanadamu haijafika kikomo; kazi hiyo itamalizika tu wakati mwanadamu amesafishwa kikamilifu, wakati wale ambao wamejikabidhi kwa Mungu kikweli wamekamilishwa, na wakati wale wadanganyifu wasiokuwa na Mungu ndani ya mioyo yao wamesafishwa. Wale ambao hawamridhishi Mungu katika hatua ya mwisho ya kazi Yake wataondolewa kabisa, na wale watakaooondolewa kabisa ni wa yule mwovu. Kwa kuwa hawawezi kumtosheleza Mungu, wao ni waasi dhidi ya Mungu, na hata kama watu hawa wanamfuata Mungu leo, hili si thibitisho kwamba wao ndio watakaosalia mwisho. Kwa maneno mengine “wale ambao humfuata Mungu hadi mwisho watapokea wokovu,” maana ya “kufuata”

ni kusimama imara katikati ya taabu. Leo, wengi wanaamini kwamba kumfuata Mungu ni rahisi, lakini wakati kazi ya Mungu inakaribia kuisha, utajua maana halisi ya “kufuata.” Kwa sababu tu kwamba unaweza kumfuata Mungu leo baada ya kushindwa, si thibitisho kwamba umo miongoni mwa wale watakaokamilishwa. Wale wasioweza kustahimili majaribu, wale wasioweza kuwa washindi wakiwa kwenye taabu, hatimaye, wataashindwa kusimama imara, na basi kushindwa kumfuata Mungu hadi mwisho kabisa. Wale wanaomfuata Mungu kiukweli wana uwezo wa kuhimili majaribu ya kazi yao, ilhali wale wasiomfuata hawawezi kuhimili majaribu yoyote ya Mungu. Karibuni au baadaye watatimuliwa, huku washindi wakisalia kwenye ufalme. Mwanadamu amtafute au asimtafute Mungu kwa ukweli itapimwa kulingana na kazi yake, yaani, kupitia kwa majaribu ya Mungu na hayahusiani na uamuzi wa mwanadamu mwenyewe. Mungu hamkatai mtu yeyote kwa wazo la ghafla; yote ambayo Yeye hufanya yanaweza kumshawishi binadamu kikamilifu. Haya ni lolote ambalo halionekani kwa mwanadamu ama kazi yoyote ambayo haiwezi kumthibitishia mwanadamu. Iwapo imani ya mwanadamu ni ya ukweli au sio huthibitishwa na ushahidi, na haiwezi kuamuliwa na mwanadamu. Kwamba “ngano haiwezi kufanywa magugu, na magugu hayawezi kufanywa ngano” ni jambo lililo wazi. Wale wote wanaompenda Mungu kwa dhati hatimaye watasalia katika ufalme, na Mungu hatamtesa yeyote ambaye Yeye anampenda kwa kweli. Kwa misingi ya kazi zao na shuhuda zao tofauti, washindi katika ufalme watatumika kama makuhani au wafuasi, na wale wote watakaoshinda taabu watakuwa mwili wa makuhani katika ufalme. Baraza la makuhani litaundwa wakati kazi ya injili ulimwenguni kote itafikia kikomo. Wakati huo ukitimia, yale yanayopaswa kufanywa na mwanadamu yatakuwa jukumu lake ndani ya ufalme wa Mungu, na kuishi kwake pamoja na Mungu katika ufalme. Katika baraza la makuhani, patakuwepo makuhani wakuu na makuhani, na watakaosalia watakuwa wana na watu wa Mungu. Haya yote huamuliwa na ushuhuda wao kwa Mungu wakati wa majaribu; sio nyadhifa zinazopeanwa kwa wazo la ghafla. Wakati hadhi ya mwanadamu itakuwa imeianzishwa, kazi ya Mungu itamalizika, kwa kuwa kila mojawapo imewekwa kulingana na aina yake na kurejeshwa katika hali yake halisia, na hii ndiyo alama ya ukamilisho wa kazi ya Mungu, na haya ndiyo matokeo ya mwisho ya kazi ya Mungu na matendo ya mwanadamu, na ndiko kubainika kwa yale maono ya kazi ya Mungu na ushirikiano wa mwanadamu. Mwishowe, mwanadamu atapata pumziko katika ufalme wa Mungu, na, Mungu pia, atarejea kwenye makazi Yake kupumzika. Haya ndiyo yatakayokuwa matokeo ya miaka 6,000 ya ushirikiano wa mwisho kati ya Mungu na mwanadamu.

Kiini Cha Kristo Ni Utiifu kwa Mapenzi ya Baba wa Mbinguni

Mungu mwenye mwili Anaitwa Kristo, na Kristo ni mwili uliovishwa na Roho wa Mungu. Mwili huu ni tofauti na wa mwanadamu yeyote aliye wa nyama. Tofauti hii ni kwa sababu Kristo

sio wa mwili na damu bali ni mwili wa Roho. Anao ubinadamu wa kawaida na uungu kamili. Uungu Wake haujamilikiwa na mwanadamu yeyote. Ubinadamu Wake wa kawaida unaendelea shughuli Zake zote za kawaida katika mwili, wakati uungu Wake unafanya kazi ya Mungu Mwenyewe. Basi iwe ubinadamu Wake au uungu, yote hujiwasilisha kwa mapenzi ya Baba wa mbinguni. Kiini cha Kristo ni Roho, yaani, uungu. Kwa hivyo, chemichemi Yake ni ile ya Mungu Mwenyewe; Dutu hii haitapinga kazi Yake Mwenyewe, na Yeye hangeweza kufanya kitu chochote kinachoharibu kazi Yake Mwenyewe, wala milele Yeye kutamka maneno yoyote ambayo yanakwenda kinyume na mapenzi Yake Mwenyewe. Kwa hiyo, Mungu mwenye mwili kamwe hangefanya kazi yoyote ambayo inasumbua usimamizi Wake Mwenyewe. Hili ndilo ambalo binadamu wote wanapaswa kuelewa. Kiini cha kazi ya Roho Mtakatifu ni kuokoa binadamu na ni kwa ajili ya usimamizi wa Mungu Mwenyewe. Vile vile, kazi ya Kristo ni kuokoa binadamu na ni kwa ajili ya mapenzi ya Mungu. Kutokana na kwamba Mungu Anapata mwili, Anatambua dutu Yake ndani ya mwili Wake, kama kwamba mwili Wake ni wa kutosha kufanya kazi Yake. Kwa hivyo, kazi zote za Roho wa Mungu zinabadilishwa na kazi ya Kristo wakati wa kupata mwili, na kwenye msingi wa kazi zote wakati wa kupata mwili ni kazi ya Kristo. Haiwezi kuchanganyika na kazi yoyote ile kutoka enzi nyingine yoyote. Na kwa kuwa Mungu Anakuwa mwili, Yeye Anafanya kazi katika utambulisho wa mwili Wake; kwa kuwa Yeye hukuja katika mwili, kisha Yeye humaliza katika mwili kazi hiyo Anayoazimia kufanya. Iwe ni Roho wa Mungu au ni Kristo, wote ni Mungu Mwenyewe, na Anafanya kazi hiyo Anayoazimia kufanya na hufanya huduma hiyo Anayopaswa kufanya.

Dutu ya Mungu yenyewe hushika na kutumia mamlaka, lakini Yeye Anao uwezo wa kuwasilisha kwa ukamilifu mamlaka ambayo hutoka Kwake. Iwe ni kazi ya Roho au kazi ya mwili, hakuna ambayo itazozana na nyingine. Roho wa Mungu ndiyo mamlaka juu ya viumbe vyote. Mwili na dutu ya Mungu pia inayo mamlaka, bali Mungu katika mwili Anaweza kufanya kazi yote inayotii mapenzi ya Baba wa mbinguni. Hii haiwezi kupatikana au kufanyika na binadamu yeyote. Mungu Mwenyewe ni mamlaka, lakini mwili Wake unaweza kunyenyekea kwa mamlaka Yake. Hii ndiyo maana ya ndani ya maneno: “Kristo hutii mapenzi ya Mungu Baba.” Mungu ni Roho na Anaweza kufanya kazi ya wokovu, kama vile Mungu Anavyoweza kuwa mwanadamu. Hata hivyo, Mungu Mwenyewe Anafanya kazi Yake Mwenyewe; Yeye wala hazuii wala kuathiri, wala kufanya kazi inayozipinganisha pande zote mbili, kwa kuwa kiini cha kazi iliyofanywa na Roho na mwili yote ni sawa. Iwe ni Roho au mwili, vyote hufanya kazi kutimiza nia moja na kusimamia kazi sawa. Ingawa Roho na mwili huwa na sifa mbili tofauti, dutu yao ni sawa; zote zina dutu ya Mungu Mwenyewe, na utambulisho wa Mungu Mwenyewe. Mungu Mwenyewe hana mambo ya kuasi; dutu Yake ni nzuri. Yeye ni udhihirisho wa uzuri wote na wema, vile vile upendo wote. Hata katika mwili, Mungu hafanyi lolote linalomuasi

Mungu Baba. Hata kwa gharama ya kutoa sadaka maisha Yake, Angekuwa kwa ukamilifu tayari na kutofanya uchaguzi mwingine. Mungu hana mambo ya ukamilifu wa kibinafsi na umuhimu wa kibinafsi, au yale wa kujiona na kiburi; Hana mambo yasiyo aminifu. Yote yanayomuasi Mungu yanatoka kwa Shetani; Shetani ni chanzo cha ubaya na uovu wote. Sababu kwamba mwanadamu anayo sifa sawa na zile za Shetani ni kwa sababu mwanadamu amelaghaiwa na kushughulikiwa na Shetani. Kristo hajawahi kupotoshwa na Shetani, hivyo Anazo tu tabia za Mungu na hakuna hata moja ya Shetani. Haijalishi ugumu wa kazi, au udhaifu wa mwili, Mungu, wakati Anapoishi katika mwili, kamwe hatafanya kitu chochote kitakachopinga kazi ya Mungu Mwenyewe, wala kuacha mapenzi ya Mungu Baba kwa njia ya uasi. Ni afadhali Ateseke maumivu ya mwili kuliko kwenda kinyume na matakwa ya Mungu Baba; ni kama vile Yesu Alisema katika sala, “Baba, kama inawezekana, kikombe hiki kiniondokee: hata hivyo si kama Mimi Nipendavyo, bali kama Wewe upendavyo.” Wanadamu watachagua, bali Kristo hawezi. Ingawa Anao utambulisho wa Mungu Mwenyewe, bado Yeye Anatafuta mapenzi ya Mungu Baba, na Anatimiza kile Alichokabidhiwa na Mungu Baba, kutoka kwa mtazamo wa mwili. Hili ni jambo ambalo haliwezi kupatikana kwa binadamu. Hilo ambalo huja kutoka kwa Shetani haliwezi kuwa na dutu ya Mungu, bali mojawapo ya yale ambayo hukosa kutii na kumpinga Mungu. Haliwezi kumtii Mungu kikamilifu, wala kutii mapenzi ya Mungu kwa hiari. Wanadamu wote isipokuwa Kristo wanaweza kufanya yaliyo ya kumpinga Mungu, na hakuna anayeweza moja kwa moja kufanya kazi aliyoaminiwa na Mungu; hakuna hata mmoja aliye na uwezo wa kuzingatia usimamizi wa Mungu kama wajibu wake wenyewe kutekeleza. Kuwasilisha mapenzi ya Mungu Baba ni kiini cha Kristo; uasi dhidi ya Mungu ni tabia ya shetani. Sifa hizo mbili hazipatani, na yeyote aliye na sifa za shetani hawezi kuitwa Kristo. Sababu ambayo binadamu hawezi kufanya kazi ya Mungu kwa niaba Yake ni kwa sababu mwanadamu hana kiini chochote cha Mungu. Binadamu humfanyia Mungu kazi kwa ajili ya maslahi binafsi ya binadamu na ya matarajio Yake ya baadaye, lakini Kristo Anafanya kazi ya kufanya mapenzi ya Mungu Baba.

Ubinadamu wa Kristo unaongozwa na uungu Wake. Ingawa yuko katika mwili, ubinadamu Wake si kama ule wa binadamu wa mwili kabisa. Anao upekee wa tabia Yake Mwenyewe, na hii pia huongozwa na uungu Wake. Uungu Wake hauna udhaifu; udhaifu wa Kristo unaelezea ule wa ubinadamu Wake. Kwa kiasi fulani, udhaifu huu huzuia uungu Wake, lakini mipaka hiyo ipo tu kati ya wigo fulani na wakati, na sio zisizo na mipaka. Linapokuja suala la muda wa kufanya kazi ya uungu Wake, hufanyika bila kujali ubinadamu Wake. Ubinadamu wa Kristo kabisa huongozwa na uungu Wake. Mbali na maisha ya kawaida ya ubinadamu Wake, matendo mengine yote ya ubinadamu Wake ni ya kushawishiwa, inayoathirika na kuelekezwa na uungu Wake. Ingawa Kristo Anao ubinadamu, haukatizi kazi ya uungu Wake. Hii hasa ni kwa sababu ubinadamu wa Kristo unaongozwa na uungu Wake; ingawa ubinadamu Wake haujakomaa katika

mwenendo Wake mbele ya wengine, hauathiri kazi ya kawaida ya uungu Wake. Ninaposema kwamba ubinadamu Wake haujapotoshwa, Ninamaanisha kwamba ubinadamu wa Kristo unaweza moja kwa moja kuongozwa na uungu Wake, na kwamba Yeye ni mwenye hisia kubwa kuliko ile ya mwanadamu wa kawaida. Ubinadamu Wake unafaa zaidi kwa kuongozwa na uungu katika kazi Yake; ubinadamu Wake una uwezo wa kuonyesha kazi ya uungu, kama vile unao uwezo wa kutii kazi kama hiyo. Mungu Anapofanya kazi katika mwili, hajawahi kamwe kupoteza maono ya wajibu wa mwanadamu katika mwili Anaopaswa kutimiza; Anao uwezo wa kumwabudu Mungu mbinguni kwa moyo wa kweli. Anayo dutu ya Mungu, na utambulisho Wake ni mfano wa Mungu Mwenyewe. Ni kwamba tu Amekuja duniani na kuwa kiumbe aliyeumbwa, na ganda la nje la kiumbe, na sasa Amemiliki ubinadamu ambao hakuwa nao mwanzo; Yeye anao uwezo wa kumwabudu Mungu mbinguni. Hiki ni kiumbe cha Mungu Mwenyewe na hakiigwi na binadamu. Utambulisho Wake ni Mungu Mwenyewe. Ni kutokana na mtazamo wa mwili ndio Yeye huabudu Mungu; Kwa hivyo, maneno “Kristo huabudu Mungu mbinguni” si kwa makosa. Kile Anachouliza binadamu hasa ni nafsi Yake Mwenyewe; Yeye tayari Ameshafanikisha yote Anayotarajia kutoka kwa binadamu kabla ya kuwauliza wafanye hayo. Asingeweza kudai wengine wakati Yeye Mwenyewe Anapata kwao bure, kwa kuwa haya yote yanayotengeneza nafsi Yake. Bila kujali jinsi Yeye hufanya kazi Yake, wala Naye hangewahi kutenda kwa namna inayomuasi Mungu. Haijalishi Analomuuliza mwanadamu, hakuna mahitaji Yake yanayozidi uwezo wa mwanadamu kupata. Yote Afanyayo ni kufanya mapenzi ya Mungu na ni kwa ajili ya usimamizi Wake. Uungu wa Kristo ni zaidi ya wanadamu wote, kwa hivyo Yeye Anayo mamlaka ya juu ya viumbe vyote vilivyoundwa. Mamlaka haya ni uungu Wake, yaani, nafsi na tabia ya Mungu Mwenyewe, ambayo huamua utambulisho Wake. Kwa hiyo, haijalishi jinsi ubinadamu Wake ni wa kawaida ni wazi kuwa Anao utambulisho wa Mungu Mwenyewe; haijalishi upande Anaosimama Akiongea na kwa vyovyote vile Yeye hutii mapenzi ya Mungu, haiwezi kusemwa kwamba Yeye si Mungu Mwenyewe. Wanadamu wajinga na wapumbavu mara nyingi huchukua ubinadamu wa kawaida wa Kristo kama dosari. Haijalishi jinsi Anavyofichua na kuonyesha nafsi ya uungu Wake, mwanadamu bado hawezi kukiri kwamba Yeye ni Kristo. Na zaidi kwamba Kristo Anaonyesha utii Wake na unyenyekevu, ndivyo wanadamu wengi wajinga humchukua Kristo kwa mzaha. Kuna hata wale ambao huelekeza Kwake mtizamo wa kutengwa na dharau, ilhali kuweka wale “wanadamu wakubwa” wa picha ya kujidai juu ya meza na kuwaabudu. Upinzani wa binadamu dhidi ya, na uasi wa Mungu huja kutokana na ukweli kwamba kiini cha Mungu mwenye mwili hutii mapenzi ya Mungu, vile vile kutokana ubinadamu wa kawaida wa Kristo; hapa ndipo kuna chanzo cha upinzani wa binadamu na uasi wake kwa Mungu. Kama Kristo hangekuwa mwenye umbo la ubinadamu wala nia ya kutafuta mapenzi ya Mungu Baba kutoka katika mtazamo wa kiumbe aliyeumbwa, lakini badala yake kumiliki ubinadamu mkuu, basi kuna uwezekano hakungekuwa

na uasi katika mwanadamu yeyote. Sababu ya binadamu kuwa tayari kuamini katika Mungu Asiyeonekana mbinguni ni kwa sababu Mungu mbinguni hana ubinadamu na Yeye hana sifa ya kiumbe hata moja. Hivyo binadamu siku zote humchukua Yeye kwa heshima kubwa, lakini anayo tabia ya dharau kwa Kristo.

Ingawa Kristo duniani Anaweza kufanya kazi kwa niaba ya Mungu Mwenyewe, hajakuja na nia ya kuonyesha watu wote mfano Wake katika mwili. Yeye hajakuja kwa watu wote kumwona; Anakuja kwa ajili ya kuwaruhusu binadamu kuongozwa na mkono Wake, na hivyo kuingia katika enzi mpya. Kazi ya mwili wa Kristo ni kwa ajili ya kazi ya Mungu Mwenyewe, yaani, kwa ajili ya kazi ya Mungu katika mwili, na si ili kuwawezesha binadamu kuelewa kikamilifu kiini cha mwili Wake. Haijalishi jinsi Anavyofanya kazi, haiwezi kuzidi yanayoweza kupatwa na mwili. Haijalishi jinsi Anavyofanya kazi, anafanya hivyo katika mwili na ubinadamu wa kawaida, na wala hafichui kwa kikamilifu kwa mwanadamu uso wa kweli wa Mungu. Zaidi ya hayo, kazi Yake katika mwili kamwe sio isiyo ya kawaida au isiyokadirika kama mwanadamu anavyodhani. Japokuwa Kristo Anamwakilisha Mungu Mwenyewe katika mwili na hufanya binafsi ambayo Mungu Mwenyewe Anapaswa kufanya, Yeye hakani kuwepo kwa Mungu mbinguni, wala kuyatangaza matendo Yake Mwenyewe kwa msisimko. Badala yake, Yeye kwa unyenyekevu Hubaki kwa siri ndani ya mwili Wake. Mbali na Kristo, wale ambao wanadai kwa udanganyifu kuwa Kristo hawana sifa Zake. Wakiwekwa sambamba dhidi ya tabia za kiburi na kujiinua za Kristo wa uongo, inakuwa dhahiri aina gani ya mwili ndiye Kristo wa kweli. Walivyo waongo zaidi, ndivyo Kristo wa uongo wanavyojionyesha wenyewe, na ndivyo wanavyoweza zaidi kufanya kazi za ishara na maajabu ya kuwahadaa binadamu. Kristo wa uongo hawana sifa za Mungu; Kristo hajachafuliwa na kipengele chochote cha dutu ya Kristo wa uongo. Mungu hupata mwili tu kukamilisha kazi ya mwili, na sio tu kuwaruhusu watu wote kumwona. Badala yake, Yeye huacha kazi Yake ithibitishe utambulisho Wake, na kuruhusu Anachofichua kushuhudia dutu Yake. Dutu Yake haikosi msingi; utambulisho Wake haukukamatwa na mkono Wake; huamuliwa kwa kazi Yake na dutu Yake. Ingawa Anacho kiini cha Mungu Mwenyewe na uwezo wa kufanya kazi ya Mungu Mwenyewe, Yeye bado, hata hivyo, mwili ambao sio kama Roho. Yeye si Mungu na sifa za Roho; Yeye ni Mungu na ganda la mwili. Kwa hivyo, haijalishi jinsi ya ukawaida Wake na Alivyo mdhaifu, na vyovyote vile Anavyotafuta mapenzi ya Mungu Baba, uungu Wake ni usioweza kupingwa. Katika mwili wa Mungu haupo tu ubinadamu wa kawaida na udhaifu Wake; kuna hata zaidi uzuri na mambo yasiyoeleweka ya uungu Wake, na vile vile matendo Yake yote katika mwili. Kwa hiyo, ubinadamu na uungu kwa kweli vipo kwa matendo ndani ya Kristo. Hili sio jambo tupu au lisilo la kawaida kwa vyovyote vile. Yeye huja duniani na lengo kuu la kufanya kazi; ni muhimu kumiliki ubinadamu wa kawaida kutekeleza kazi duniani; la sivyo, haijalishi ukubwa wa nguvu

ya uungu Wake, kazi Yake ya awali haiwezi kutiwa katika utumizi mzuri. Ingawa ubinadamu Wake ni wa umuhimu mkubwa, sio dutu Yake. Dutu Yake ni uungu; Kwa hiyo, wakati Anapoanza kufanya huduma Yake hapa duniani ndio wakati Yeye huanza kuonyesha nafsi ya uungu Wake. Ubinadamu Wake uko kwa ajili tu ya kuendeleza maisha ya kawaida ya mwili Wake ili uungu Wake uweze kufanya kazi kama kawaida katika mwili; ni uungu ndio unaoongoza kazi Yake kwa ukamilifu. Wakati Anapomaliza kazi Yake, Atakuwa Ametimiza mujibu wa huduma Yake. Wanachopaswa kujua wanadamuni ni ukamilifu wa kazi Yake, na ni kwa njia ya kazi Yake kuwa Yeye Humwezesha binadamu kumjua Yeye. Katika kipindi cha kazi Yake, Yeye huonyesha kikamilifu kabisa nafsi ya uungu Wake, ambayo si tabia iliyochafuliwa na ubinadamu, au nafsi iliyochafuliwa na mawazo na tabia za binadamu. Wakati utakapokuja ambapo huduma Yake yote imefika mwisho, Atakuwa tayari kwa kikamilifu na kikamilifu Amekwishaonyesha tabia hiyo Anayopaswa kueleza. Kazi Yake haifundishwi na mwanadamu yeyote; maonyesho ya tabia Yake pia ni huru kabisa, haudhibitiwi na akili au kutengenezwa na mawazo, bali hujitokeza kiasili. Hili haliwezi kutimizwa na binadamu yeyote. Hata kama mazingira ni magumu au hali haziruhusu, Yeye Anao uwezo wa kuonyesha tabia Yake kwa wakati muafaka. Yule Ambaye ni Kristo Anaonyesha nafsi ya Kristo, ilhali wale ambao sio hawana tabia za Kristo. Kwa hivyo, hata kama wote watampinga Yeye au kuwa na fikira Kwake, hakuna anayeweza kukana kwa misingi ya fikira ya mwanadamu kwamba tabia iliyoonyeshwa na Kristo ni ile ya Mungu. Wale wote ambao humfuata Kristo kwa moyo wa kweli au kumtafuta Mungu kwa nia watakubali kwamba Yeye ni Kristo kulingana na maonyesho ya uungu Wake. Wao kamwe hawangewahi kumkataa Kristo kwa misingi ya kipengele chochote Chake ambacho hakipatani na fikira za mwanadamu. Ingawa binadamu ni wapumbavu sana, wote wanajua hasa ni nini mapenzi ya binadamu na kile kitokacho kwa Mungu. Ni kwamba tu watu wengi kwa makusudi humpinga Kristo kutokana na makusudi yao wenyewe. Kama si kwa ajili ya haya, hakuna hata mwanadamu mmoja angekuwa na sababu ya kukataa kuwepo kwa Kristo, kwa kuwa uungu uliodhihirishwa na Kristo kwa hakika upo, na kazi Yake inaweza kushuhudiwa kwa macho ya wote.

Kazi na maonyesho ya Kristo huamua dutu Yake. Yeye Anaweza kukamilisha kwa moyo wa kweli kile Alichuaminiwa kufanya. Anaweza kumwabudu Mungu mbinguni kwa moyo wa kweli, na kwa moyo wa kweli Atafute mapenzi ya Mungu Baba. Yote haya yanaamuliwa na dutu Yake. Na vile vile ufunuo Wake wa asili pia unaamuliwa na dutu Yake; sababu ya ufunuo Wake wa asili kuitwa hivyo ni kwa sababu ya maonyesho Yake siyo maigizo, au matokeo ya elimu na mwanadamu, au matokeo ya miaka mingi ya kukuzwa na mwanadamu. Hakujiifunza au kujivika nayo Yeye Mwenyewe; badala yake, ni asili ndani Yake. Mwanadamu anaweza kukataa kazi Yake, maonyesho Yake, ubinadamu Wake, na maisha yote ya ubinadamu Wake wa kawaida,

lakini hakuna hata mmoja anayeweza kukana kwamba Yeye humwabudu Mungu mbinguni kwa moyo wa kweli; hakuna anayeweza kukana kwamba Amekuja kutimiza mapenzi ya Baba wa mbinguni, na hakuna anayeweza kukana uaminifu Alio nao Anapomtafuta Mungu Baba. Ingawa mfano Wake si wa kupendeza hisia, ingawa hotuba Yake haujajawa na hewa ya ajabu, na kazi Yake sio ya kutikisa ulimwengu au mbingu vile mwanadamu anavyofikiria, Yeye hakika ni Kristo, Anayetimiza mapenzi ya Baba wa mbinguni kwa moyo wa kweli, Ananyenyekea kikamilifu kwa Baba wa mbinguni, na ni mtiifu mpaka wakati kifo. Hii ni kwa sababu dutu Yake ni dutu ya Kristo. Ukweli huu ni mgumu kwa mwanadamu kuamini lakini kwa kweli upo. Wakati huduma ya Kristo imetimia kikamilifu, mwanadamu ataweza kuona kutokana na kazi Zake kwamba tabia Yake na nafsi Yake yanawakilisha tabia na nafsi ya Mungu huko mbinguni. Wakati huo, ujumla wa kazi Zake zote utaweza kuthibitisha kwamba Yeye kweli ni Neno linalogeuka mwili, na si sawa na ule wa mwili na damu ya mwanadamu. Kila hatua ya kazi ya Kristo duniani ina umuhimu wakilishi Wake, lakini mwanadamu anayepitia kazi halisi ya kila hatua hawezi kufahamu umuhimu wa kazi Yake. Hii hasa ni vile katika hatua kadhaa za kazi zilizotekelezwa na Mungu katika kupata Kwake mwili mara ya pili. Wengi wa wale ambao wamesikia tu au kuona maneno ya Kristo tu lakini bado hawajawahi kumwona hawana fikira ya kazi Yake; wale ambao wamemwona Kristo na kusikia maneno Yake, na vile vile kupitia kazi Yake, huona ugumu kuikubali kazi Yake. Je, hii si kwa sababu ya kwamba kuonekana na ubinadamu wa kawaida kwa Kristo hakulingani na matarajio ya binadamu? Wale wanaokubali kazi Yake baada ya Kristo kwenda hawatakuwa na matatizo kama hayo, kwa kuwa wao wanaikubali kazi Yake na wala hawapati kukutana na ubinadamu wa kawaida wa Kristo. Mwanadamu hawezi kuacha fikira zake kuhusu Mungu na badala yake humchunguza kwa mkazo; hii ni kutokana na ukweli kwamba mwanadamu analenga tu juu ya kuonekana Kwake na anashindwa kutambua dutu Yake kwa kuzingatia kazi Yake na maneno Yake. Iwapo mwanadamu ataufumbia macho kuonekana kwa Kristo au kuepuka kujadili ubinadamu wa Kristo, na aongee tu juu ya uungu Wake, Ambao kazi Yake na maneno hayawezi kufikiwa na mwanadamu yeyote, basi fikira ya binadamu itapungua kwa nusu, hata kwa kiasi kwamba matatizo yote ya mwanadamu yatatatuliwa. Wakati wa kazi ya Mungu mwenye mwili, mwanadamu hawezi kumvumilia na amejaa wingi wa fikira mbalimbali kumhusu, na matukio ya upinzani na uasi ni kawaida. Binadamu hawezi kuvumilia kuwepo kwa Mungu, kuonyesha “upole” kwa unyenyekevu na kujificha kwa Kristo, au “kuisamehe” dutu ya Kristo inayomtii Baba wa mbinguni. Kwa hivyo, Hawezi kukaa na mwanadamu milele baada ya kumaliza kazi Yake, kwa kuwa mwanadamu hana nia ya kumruhusu kuishi pamoja nao. Iwapo mwanadamu hawawezi “kuonyesha upole” Kwake katika kipindi Chake cha kazi, basi, ni jinsi gani wangeweza kumvumilia Yeye kuishi nao baada ya kumaliza kutekeleza shughuli Zake, kuwaangalia hatua kwa hatua na wakipitia maneno Yake? Je, si wengi kisha wangeanguka kwa

ajili Yake? Mwanadamu anamruhusu tu kufanya kazi duniani; hiki ndicho kiasi kikubwa zaidi cha upole wa mwanadamu. Kama si kwa sababu ya kazi Yake, mwanadamu angekuwa ameshamtupa nje ya dunia, hivyo kwa kiasi gani kidogo wangeweza kumwonyesha upole mara kazi Yake inapokamilika? Basi si mwanadamu angemuua na kumtesa hadi kufa? Iwapo Yeye hangekuwa Anaitwa Kristo, basi kuna uwezekano hangewahi kufanya kazi miongoni mwa wanadamu; iwapo Hangefanya kazi na utambulisho wa Mungu Mwenyewe, na badala yake Afanye kazi tu kama mwanadamu wa kawaida, basi mwanadamu hangevumilia Yeye kutamla sentensi hata moja, wala kuvumilia hata kiasi kidogo cha kazi Yake. Basi Anaweza kubeba tu utambulisho huu pamoja Naye katika kazi Yake. Kwa njia hii, kazi Yake ni ya nguvu zaidi kuliko kama hangefanya hivyo, kwa kuwa binadamu wote wako tayari kutii hadhi na utambulisho mkubwa. Iwapo Yeye hangekuwa na utambulisho wa Mungu Mwenyewe Alipokuwa akifanya kazi ama kuonekana kama Mungu Mwenyewe, basi hangekuwa na nafasi ya kufanya kazi hata kidogo. Ingawa Yeye Anayo dutu ya Mungu na nafsi ya Kristo, mwanadamu hangelegea na kumruhusu kufanya kazi kwa urahisi miongoni mwa wanadamu. Yeye hubeba utambulisho wa Mungu Mwenyewe katika kazi Yake; ingawa kazi hiyo ina nguvu mara kadhaa zaidi kuliko ile hufanyika bila utambulisho huo, bado wanadamu sio watiifu Kwake kikamilifu, kwa kuwa binadamu hunyenyekea tu kwa msimamo Wake wala si dutu Yake. Kama ni hivyo, wakati labda siku moja Kristo aamue kujiuzulu kutoka katika wadhifa Wake, inawezekana mwanadamu amruhusu kubaki hai hata kwa siku moja? Mungu yuko tayari kuishi duniani na binadamu ili Aweze kuona matokeo ambayo kazi ya mikono Yake italetika katika miaka itakayofuata. Hata hivyo, binadamu wanashindwa kuvumilia kukaa Kwake duniani hata siku moja, hivyo inamfanya kukata tamaa. Tayari ni kiasi kikubwa cha upole na neema ya mwanadamu kumruhusu Mungu kutenda kazi Anayopaswa kufanya miongoni mwa wanadamu na kutimiza huduma Yake. Ingawa wale ambao wameshindwa kibinafsi na Yeye wanamwonyesha neema kuu, bado tu wamempa kibali cha kuwepo tu kwa ajili ya kutimiza kazi Yake na si hata saa moja zaidi baada ya kukamilisha kazi hiyo. Iwapo ni hivyo, je itakuwaje na wale ambao bado hawajashindwa na yeye? Je, sababu ambayo mwanadamu anamtendea Mungu mwenye mwili kwa njia hii ni kwa sababu Yeye ni Kristo na ganda la binadamu wa kawaida? Iwapo Angekuwa tu na uungu na sio ubinadamu wa kawaida, basi si matatizo ya binadamu yangetatuliwa kwa urahisi mno? Binadamu kishingo upande anatambua uungu Wake na haonyeshi haja yoyote katika ganda Lake la ubinadamu wa kawaida, licha ya ukweli kwamba dutu Yake ni sawa hasa kama vile ile ya Kristo inayonyenyekea kwa mapenzi ya Baba wa mbinguni. Kwa sababu hii, Aliweza tu kuikomesha kazi Yake ya kuwa miongoni mwa wanadamu kushiriki pamoja nao katika furaha na huzuni, kwa kuwa mwanadamu hangeweza tena kuvumilia uwepo Wake.

Kurejesha Maisha ya Kawaida ya Mwanadamu na Kumpeleka Kwenye Hatima ya Ajabu

Mwanadamu anaelewa sehemu ndogo ya kazi ya leo na kazi ya baadaye, lakini hafahamu hatima ambapo mwanadamu ataingia. Kama kiumbe, mwanadamu anapaswa kutekeleza wajibu wa kiumbe: Mwanadamu anapaswa kumfuata Mungu kwa lolote afanyalo; mnapaswa muendelea mbele kwa njia yoyote ambayo Nitawaambia. Wewe huna mbinu ya kusimamia vitu mwenyewe, na huna ustadi juu yako mwenyewe; yote ni lazima yaachwe kwa rehema za Mungu, na kila kitu kinashikiliwa katika mikono Yake. Kama kazi ya Mungu ilimkimu mwanadamu kwa kumpa hatima, hatima ya ajabu, kabla ya wakati, na kama Mungu alitumia hii kumshawishi mwanadamu na kusababisha mwanadamu kumfuata Yeye—kama Yeye alifanya mpango na mwanadamu—basi huu haungekuwa ni ushindi, wala haingekuwa kufanya kazi katika maisha ya binadamu. Kama Mungu angetumia hatima ya mambo kumtawala au kumdhibiti mwanadamu na kupata moyo wake, basi kwa hii Hangekuwa anamkamilisha mwanadamu, wala Hangeweza kumpata mwanadamu, lakini badala yake angekuwa akitumia hatima kumdhibiti. Mwanadamu anajali tu kuhusu hatima ya siku zijazo, hatima, na kama kuna ama hamna kitu kizuri cha kutumainia. Iwapo mwanadamu angepewa matumaini mazuri wakati wa kazi ya ushindi, na kama, kabla ya kushindwa kwa mwanadamu, yeye angepewa hatima ifaayo ya kufuata, basi kushindwa kwa mwanadamu kusingekosa kuwa na athari tu, bali athari za kushindwa zingeshawishika pia. Hivi ni kusema kwamba, kazi ya ushindi inafanikisha mazao yake kwa kuchukua hatima na matarajio ya mwanadamu na kuhukumu na kuadibu uasi wa tabia ya mwanadamu. Haifanikishwi kwa kufanya mpango na mwanadamu, yaani, kwa kumpa mwanadamu baraka na neema, lakini ni kwa kufichua uaminifu wa mwanadamu kwa kumnyang'anya “uhuru” wake na kukomesha matarajio yake. Hiki ni kiini cha kazi ya ushindi. Kama mtu angepewa matumaini mazuri hapo mwanzoni sana, na kazi ya kuadibu na hukumu zingefanywa baadaye, basi mwanadamu angekubali kuadibu huku na hukumu kwa msingi kwamba alikuwa na matarajio, na mwishowe, utiifu na ibada ya Muumba isiyo na masharti ya viumbe vyote vyake haingetimizika; kungekuwepo tu na utiifu wenye upofu na wa ujinga, au pengine mwanadamu angetoa madai yasiyo na msingi kwa Mungu, na ingekuwa ni vigumu kushinda moyo wa mwanadamu. Kwa hivyo, kazi kama hii ya ushindi haingekuwa na uwezo wa kumpata mwanadamu, wala, zaidi ya hayo, ya kuwa na ushuhuda kwa Mungu. Viumbe kama hawa hawangeweza kutekeleza jukumu lao, na wangeweza tu kufikia makubaliano na Mungu; hii haitakuwa ushindi, lakini huruma na baraka. Tatizo kubwa mno kwa mwanadamu ni kuwa yeye hufikiria tu kuhusu hatima yake na matarajio, na kuyaabudu. Mwanadamu humfuata Mungu kwa ajili ya hatima yake na matarajio; yeye hamwabudu Mungu kwa sababu ya upendo wake kwake. Na kwa hivyo, katika ushindi kwa mwanadamu, ubinafsi wa mwanadamu, uroho

na vitu ambavyo sana sana huzuia ibada yake kwa Mungu ni sharti vishughulikiwe na hapo viondolewe. Kwa kufanya hivyo, matokeo ya ushindi kwa mwanadamu yatatimizwa. Hivyo, katika ushindi wa kwanza wa mwanadamu ni muhimu kuondoa matarajio makubwa na udhaifu mkubwa kabisa wa mwanadamu, na, kupitia hili, kufichua upendo wa mwanadamu kwa Mungu, na kubadilisha maarifa yake kuhusu maisha ya binadamu, mtazamo wake kwa Mungu, na maana ya kuwepo kwake. Kwa njia hii, upendo wa mwanadamu kwa Mungu unatakaswa, ambapo ni kusema, moyo wa binadamu unashindwa. Lakini katika mtazamo wake wa viumbe vyote, Mungu hashindi kwa sababu ya kushinda; badala yake, Yeye anashinda ili kumpata mtu, kwa sababu ya utukufu wake mwenyewe, na ili kuokoa ufanano wa kwanza wa awali wa mwanadamu. Kama angeshinda kwa ajili ya kushinda, basi umuhimu wa kazi ya ushindi ungepotea. Hiyo ni kusema kuwa ikiwa, baada ya kumshinda mwanadamu, Mungu alikata tamaa kwa ajili ya mwanadamu, na hakuzingatia maisha au kifo chake, basi hii haitakuwa usimamizi wa mwanadamu, wala kumshinda mwanadamu haitakuwa ni kwa ajili ya wokovu wake. Ni upato wa mwanadamu tu kufuatia ushindi wake na ujio wake wa mwisho katika hatima ya ajabu ndiyo yaliyomo katika kiini cha kazi yote ya wokovu, na ni hii tu ndio inayoweza kufikia lengo la wokovu wa mwanadamu. Kwa maneno mengine, ni ufikaji wa mwanadamu katika hatima nzuri na kuingia kwake katika mapumziko tu ndiyo matarajio ambayo yanatakiwa yamilikiwe na viumbe vyote, na kazi ambayo lazima ifanywe na Muumba. Kama mwanadamu ndiye ambaye angefanya kazi hii, basi kazi hii ingekuwa kidogo sana. Ingemchukua mwanadamu hadi kiwango fulani, lakini haingekuwa na uwezo wa kumleta mwanadamu katika hatima ya milele. Mwanadamu hana uwezo wa kuamua hatima ya mwanadamu, wala, zaidi ya hayo, hana uwezo wa kuhakikisha matarajio na hatima ya baadaye ya binadamu. Kazi inayofanywa na Mungu, hata hivyo, ni tofauti. Tangu Yeye amuumbe mwanadamu, Yeye anamwongoza; kwa sababu Yeye humwokoza mwanadamu, atamwokoza mwanadamu kwelikweli, na atampata kikamilifu; kwa kuwa Yeye humwongoza mwanadamu, atamleta kwenye hatima inayofaa; na kwa kuwa Yeye alimuumba mwanadamu na humsimamia mwanadamu, ni sharti Achukue jukumu la hatima ya mwanadamu na matarajio yake. Ni hii ndio kazi ambayo hufanywa na Muumba. Ingawa kazi ya ushindi inatimizwa kwa kutakasa matarajio ya mwanadamu, hatimaye ni lazima mwanadamu aletwe kwenye hatima ifaayo aliyotengenezewa na Mungu kwa ajili yake. Ni kwa sababu hasa kuwa Mungu hufanya kazi katika mwanadamu ndiyo maana mwanadamu ana hatima na hatima yake ni ya uhakika. Hapa, hatima ifaayo inayoangaziwa sio matumaini na matarajio yaliyotakaswa katika nyakati za zamani, hizi mbili ni tofauti. Kitu ambacho mwanadamu hutumainia na kufuata ni tamaa za harakati ya hamu ya kimwili iliyo badhirifu, badala ya hatima ya mwanadamu anayotazamiwa. Kile ambacho Mungu amemwandalia mwanadamu, wakati huo huo, ni baraka na ahadi alizoandaliwa mwanadamu mara baada ya kutakaswa, ambayo Mungu alimtayarishia mwanadamu baada ya kuumba ulimwengu, na ambayo haitiwi doa na uchaguzi,

dhana, mawazo au mwili wa mwanadamu. Hatima hii haitayarishwi kwa ajili ya mtu fulani, lakini ni mahali pa kupumzikia pa wanadamu wote. Na kwa hivyo, hii hatima ni hatima inayofaa zaidi kwa wanadamu.

Muumba anakusudia kupanga viumbe vyote. Wewe ni lazima usitupe au kutokaidi chochote ambacho Yeye anakifanya, wala usiwe na uasi kwake. Wakati ambapo kazi ambayo Yeye hufanya hatimaye inatimiza nia Yake, katika hii atapata utukufu. Leo, ni kwa nini haisemwi kwamba nyinyi ni wa uzao wa Moabu, au watoto wa joka kuu jekundu? Je, ni kwa nini hakuna mazungumzo ya wateule, na mazungumzo pekee ni ya viumbe? Kiumbe—hili lilikuwa jina la asili la mwanadamu, na ni hili ndilo utambulisho wake wa asili. Majina yanatofautiana tu kwa sababu nyakati na vipindi ni tofauti; kwa kweli, mwanadamu ni kiumbe wa kawaida. Viumbe wote, ikiwa ni wapotovu zaidi ama ni watakatifu sana, ni lazima watekeleze wajibu wa kiumbe. Wakati Yeye anafanya kazi ya ushindi, Mungu hakudhibiti kwa kutumia matarajio yako, majaliwa au hatima. Kwa kweli hakuna haja ya kufanya kazi kwa namna hii. Lengo la kazi ya ushindi ni kumfanya mwanadamu atekeleze wajibu wa kiumbe, kumfanya aabudu Muumba, na ni baada ya hii tu ndivyo ataweza kuingia kwenye hatima ya kustaajabisha. Majaliwa ya mwanadamu yanadhibitiwa na mikono ya Mungu. Wewe huna uwezo wa kujidhibiti mwenyewe: Licha ya mwanadamu yeye mwenyewe daima kukimbilia na kujishughulisha, anabakia bila uwezo wa kujidhibiti. Kama ungejua matarajio yako mwenyewe, kama ungeweza kudhibiti majaliwa yako mwenyewe, ingekuwa wewe bado ni kiumbe? Kwa kifupi, bila kujali jinsi Mungu hufanya kazi, kazi yote yake ni kwa ajili ya mwanadamu. Chukua, kwa mfano, mbingu na nchi na vitu vyote ambavyo Mungu aliviumba ili kumhudumia mwanadamu: mwezi, jua, na nyota ambazo Yeye alimuambia mwanadamu, wanyama na mimea, majira ya machipuko, majira ya joto, vuli na baridi, na kadhalika—yote yametengenezwa kwa ajili ya kuwepo kwa mwanadamu. Na kwa hivyo, bila kujali ni jinsi gani anavyoadibu na kuhukumu mwanadamu, yote ni kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Japokuwa yeye humnyang'anya mwanadamu matumaini yake ya kimwili, ni kwa ajili ya kumtakasa mwanadamu, na utakaso wa mwanadamu ni kwa ajili ya kuishi kwake. Hatima ya mwanadamu iko mikononi mwa Muumba, hivyo ni jinsi gani mwanadamu anaweza kujidhibiti mwenyewe?

Punde tu kazi ya ushindi imekwisha kamilika, mwanadamu ataletwa katika dunia nzuri. Haya maisha, bila shaka, bado yatakuwa duniani, lakini yatakuwa tofauti kabisa na jinsi maisha ya mwanadamu yalivyo leo. Ni maisha ambayo mwanadamu atakuwa nayo baada ya wanadamu kwa ujumla kushindwa, itakuwa mwanzo mpya kwa mwanadamu hapa duniani, na kwa wanadamu kuwa na maisha kama hii ni ushahidi kwamba wanadamu wameingia katika milki jipya na nzuri. Itakuwa mwanzo wa maisha ya mwanadamu na Mungu duniani. Nguzo ya maisha mema kama haya ni lazima iwe hivyo, hivi kwamba baada ya mwanadamu kutakaswa na

kushindwa, anajiwasilisha mbele za Muumba. Na kwa hivyo, kazi ya ushindi ni awamu ya mwisho ya kazi ya Mungu kabla ya wanadamu kuingia katika hatima ya ajabu. Maisha kama haya ni maisha ya baadaye ya mwanadamu duniani, ni maisha yanayopendeza zaidi duniani, aina ya maisha ambayo mwanadamu ametamania, aina ambayo mwanadamu hajawahi kamwe kutimiza katika historia ya ulimwengu. Ni matukio ya mwisho ya miaka 6,000 ya kazi ya usimamizi, na ndicho wanadamu wanatamani sana, na pia ni ahadi ya Mungu kwa mwanadamu. Lakini ahadi hii haiwezi timika mara moja: Mwanadamu ataingia katika hatima ya mbeleni punde tu kazi ya siku za mwisho zitakapokuwa zimealizika na yeye amekwisha kushindwa kikamilifu, yaani, punde tu Shetani atakapokuwa ameshindwa kabisa. Mwanadamu atakuwa hana asili ya kutenda dhambi baada ya kusafishwa, kwa sababu Mungu atakuwa amemshinda Shetani, ambayo ina maana kuwa hakutakuwepo na kuvamiwa na vikosi vya uhasama, na hakuna vikosi vya uhasama ambavyo vinaweza kushambulia mwili wa mwanadamu. Na kwa hivyo mwanadamu atakuwa huru, na mtakatifu—yeye atakuwa ameingia ahera. Ni kama tu vikosi vya uhasama wa giza vitakuwa vimefungwa ndipo mwanadamu atakuwa huru kokote aendako, na bila uasi au upinzani. Shetani ni sharti afungwe katika utumwa, and kila kitu kitakuwa sawa kwa mwanadamu; hali ya sasa ipo kwa sababu Shetani bado huchochea shida kila mahali hapa duniani, na kwa sababu kazi nzima ya usimamizi wa Mungu bado haijafika mwisho wake. Punde tu Shetani anaposhindwa, mwanadamu atakuwa amekombolewa kikamilifu; wakati mwanadamu anampata Mungu na anatoka katika kumilikiwa na Shetani, atatazama jua ya haki. Maisha atakayolipwa mwanadamu wa kawaida yatarejeshwa; yote yale ambayo ni lazima yamilikiwe na mwanadamu wa kawaida—kama uwezo wa kupambanua mema na mabaya, na kufahamu jinsi ya kula na kujivisha mwenyewe, na uwezo wa kuishi kama kawaida—yote haya yatarejeshwa. Hata kama Hawa hakuwa amejaribiwa na nyoka, mwanadamu ni lazima angekuwa na maisha kama haya ambayo ni ya kawaida baada ya kuumbwa hapo mwanzo. Ni lazima angekula, angevishwa, na kuendelea na maisha ya mwanadamu wa kawaida hapa duniani. Ila baada ya mwanadamu kupotoshwa, maisha haya yakawa ndoto, na hata leo mwanadamu hathubutu kufikiri mambo kama haya. Kwa kweli, maisha haya ya kupendeza ambayo mwanadamu anatamani ni haja yake: Iwapo mwanadamu angekuwa hana hatima kama hii, basi maisha yake ya duniani yaliyopotoshwa kamwe hayangekoma, na kama hakungekuwepo na maisha yakupendeza kama haya, basi hakungekuwa na hitimisho la majaliwa ya Shetani au kwa enzi ambayo Shetani ana utawala duniani kote. Mwanadamu ni sharti awasili kwenye ufalme ambao huwezi kufikiwa na nguvu za giza, na wakati atawasili, hii itathibitisha ya kwamba Shetani amekwisha shindwa. Kwa njia hii, punde tu hakuna usumbufu wa Shetani, Mungu mwenyewe atamdhibiti mwanadamu, na Yeye ataamuru na kudhibiti maisha yote ya mwanadamu; hii tu ndiyo itahesabika kama kushindwa kwa Shetani. Maisha ya mwanadamu leo ni sanasana maisha ya uchafu, na bado ni maisha ya kuteseka na mateso. Hii haingeitwa

kushindwa kwa Shetani; mwanadamu bado hajatoroka kutoka katika bahari ya mateso, bado hajatoroka kutoka katika ugumu wa maisha ya mwanadamu, ama ushawishi wa Shetani, na bado yeye ana maarifa ya Mungu lakini kidogo sana. Taabu zote za mwanadamu ziliumbwa na Shetani, ni Shetani ndiye alileta mateso katika maisha ya mwanadamu, na ni baada tu ya Shetani kufungwa ndipo mwanadamu ataweza kutoroka kikamilifu kutoka katika bahari ya mateso. Na bado utumwa wa Shetani unahitimika kupitia kushindwa na kupatwa kwa moyo wa mwanadamu, kwa kumfanya mwanadamu mabaki ya vita dhidi ya Shetani.

Leo, harakati ya mwanadamu ya kukuwa mshindi na kufanywa mkamilifu ni vitu ambavyo vinafuatwa kabla yeye hajakuwa na maisha ya mtu wa kawaida duniani, na ndiyo malengo ambayo mwanadamu hutafuta kabla ya utumwa wa Shetani. Kwa kiini, harakati ya mwanadamu ya kukuwa mshindi na kufanywa kamili, au kufanywa wa kutumika vilivyo, ni kutoroka kutoka katika ushawishi wa Shetani. Harakati ya mwanadamu ni kuwa mshindi, lakini matokeo ya mwisho yatakuwa ni kutoroka kutoka kwa ushawishi wa Shetani. Ni kwa kutoroka kutoka kwa ushawishi wa Shetani tu ndipo mwanadamu ataweza kuishi maisha ya mtu wa kawaida duniani, maisha ya kumwabudu Mungu. Leo, harakati ya mtu ya kukuwa mshindi na kufanywa kamilifu ndiyo mambo ambayo yanafuatwa kabla ya kuwa na maisha ya mtu wa kawaida duniani. Haya yanafuatwa kimsingi kwa ajili ya kutakaswa na kuweka ukweli katika vitendo, na ili kufanikisha ibada ya Muumba. Kama mwanadamu anamiliki maisha ya mtu wa kawaida duniani, maisha ambayo hayana taabu na matatizo, basi mwanadamu hawezi kushiriki katika harakati za kuwa mshindi. “Kuwa mshindi” na “kufanywa kamili” ni malengo ambayo Mungu humpa mwanadamu kufuatilia, na katika ufukuziaji wa malengo haya, Yeye husababisha mwanadamu kuweka ukweli katika vitendo na kuishi kwa kudhihirisha maisha yenye umuhimu. Lengo ni kumkamilisha mtu na kumpata yeye, na harakati ya kukuwa mshindi na kufanywa kamili ni njia tu. Kama, hapo mbeleni, mwanadamu ataingia kwenye hatima ya ajabu, hakutakuwepo na kurejelea kuwa mshindi na kukamilika, kutakuwepo tu na kila kiumbe kikitekeleza wajibu wake. Leo, mwanadamu anafanywa kufuata mambo haya tu ili kufafanua upeo wa mwanadamu, ili harakati ya mwanadamu ilengwe zaidi na iwe ya utendaji zaidi. La sivyo, mwanadamu angeishi katikati ya dhahania isiyo dhahiri, na kufuatilia kuingia katika uzima wa milele, na kama ingekuwa hivyo, je, si mwanadamu hata angelikuwa hafifu hata zaidi? Kufuata njia hii, bila malengo au kanuni—je, hii sio kujidanganya? Hatimaye, harakati hii ingekuwa kama kawaida bila mazao; na mwishowe, mwanadamu bado angemilikiwa na Shetani na hangeweza kujinasua mwenyewe kutokana nayo. Mbona ajikabili mwenyewe kwenye harakati kama hii isiyo na sababu? Wakati mwanadamu ataingia kwenye hatima ya milele, mwanadamu atamwabudu Muumba, na kwa sababu mwanadamu amepata wokovu na kuingia ahara, mwanadamu hawezi kimbiza malengo yoyote, wala, zaidi ya hayo, yeye hatakuwa na haja ya kuhangaika kuwa

atazingirwa na Shetani. Kwa wakati huu, mwanadamu atajua nafasi yake, na atatekeleza wajibu wake, na hata kama hataadibiwa au kuhukumiwa, kila mtu atatekeleza jukumu lake. Kwa wakati huo, mwanadamu atakuwa kiumbe katika sura na hadhi pia. Hakutakuwepo tena na tofauti ya juu na chini; kila mtu atatekeleza tu kazi tofauti. Bado mwanadamu ataishi katika hatima ya wanadamu yenye utaratibu na ifaayo, mwanadamu atatekeleza wajibu wake kwa ajili ya kumwabudu Muumba, na wanadamu kama hawa ni wanadamu wa milele. Kwa wakati huo, mwanadamu atakuwa amepata maisha yaliyoangaziwa na Mungu, maisha chini ya utunzaji na ulinzi wa Mungu, na maisha pamoja na Mungu. Wanadamu wataishi maisha ya kawaida duniani, na wanadamu wote wataingia katika njia sahihi. Mpango wa usimamizi wa miaka 6,000 utakuwa umemshinda Shetani kabisa, ambayo ina maana kuwa Mungu atakuwa amerejesha sura ya awali ya mwanadamu kufuatia kuumbwa kwake, na kwa hivyo, nia ya awali ya Mungu itakuwa imetimizwa. Hapo mwanzo, kabla mwanadamu hajapotoshwa na Shetani, mwanadamu aliishi maisha ya kawaida duniani. Baadaye, alipopotoshwa na Shetani, mwanadamu alipoteza maisha haya ya kawaida, na kwa hivyo kazi ya Mungu ya usimamizi ikaanza, na vita dhidi ya Shetani ikaanza ili kurejesha maisha ya kawaida ya mwanadamu. Ni wakati tu ambapo usimamizi wa kazi ya Mungu wa miaka 6,000 utafikia kikomo ndipo maisha ya mwanadamu yatakapoanza rasmi hapa duniani, ni wakati huo tu ndipo mwanadamu atakapokuwa na maisha mazuri, na Mungu atarejesha lengo la kumuumba mwanadamu hapo mwanzoni, na pia kufanana kwake kwa asili na mwanadamu. Na kwa hivyo, punde tu atakuwa na maisha ya kawaida ya mwanadamu duniani, mwanadamu hatafuatilia kuwa mshindi ama kuwa kamili, kwa kuwa mwanadamu atakuwa mtakatifu. “Washindi” na “kukamilishwa” ambako watu huzungumzia ni malengo yaliyopewa mwanadamu ili kufuata wakati wa vita kati ya Mungu na Shetani, na yapo tu kwa sababu mwanadamu amepotoshwa. Ni kwa kukupa lengo na kukufanya wewe kufuata lengo hili, ndipo Shetani atashindwa. Kukuambia uwe mshindi au ufanywe kamili ama utumike kunahitaji ya kwamba uwe na ushuhuda ili umwaibishe Shetani. Mwishowe, mwanadamu ataishi maisha ya mwanadamu wa kawaida duniani, na mwanadamu atakuwa mtakatifu, na wakati hii itatendeka, je, watatafuta kuwa washindi? Je, wote si viumbe wa uumbaji? Kuzungumza kuhusu kuwa mshindi na kuwa yule aliyekamilika, maneno haya yanaelekezwa kwa Shetani, na uchafu wa mwanadamu. Je, hii “mshindi” si kuhusu ushindi dhidi ya Shetani na majeshi ya uhasama? Unaposema kuwa wewe umefanywa mkamilifu, nini hicho ndani yako ambacho kimekamilishwa? Je, si kuwa umevua mwenyewe tabia potovu ya kishetani, ili uweze kufaulu kupata upendo mkuu wa Mungu? Mambo kama haya yanasemekana kuhusu mambo machafu ndani ya mtu, na kuhusu Shetani; na hayasemwi kuhusu Mungu.

Leo, kama haufuatili kuanza kuwa mshindi na kukamilishwa, basi mbeleni, wakati mwanadamu ataishi maisha ya kawaida duniani, hakutakuwa na nafasi ya harakati kama hizo.

Wakati huo, hatima ya kila aina ya mtu itakuwa imefichuliwa. Wakati huo, itakuwa wazi wewe ni kitu cha aina gani, na kama unataka kuwa mshindi au unataka kukamilishwa haitawezekana. Ni hivyo tu kwa sababu ya uasi wake mwanadamu ataadhibiwa baada ya kufichuliwa. Wakati huo, harakati za mtu hazitakuwa za juu kuliko za watu wengine, kwa wengine kuwa washindi na wengine kukamilika, au kwa wengine kuwa wazaliwa wa kwanza wa Mungu na wengine kuwa wana wa Mungu; hawatafuatilia vitu hivi. Wote watakuwa viumbe vya Mungu, wote wataishi duniani, na wote wataishi duniani pamoja na Mungu. Sasa ni wakati wa vita kati ya Mungu na Shetani, ni wakati ambapo vita hivi havijahitimishwa bado, wakati mwanadamu bado hajapatwa kikamilifu, na ni kipindi cha mpito. Na kwa hivyo, mwanadamu anatakiwa afuatilie kuwa mshindi au mmoja wa watu wa Mungu. Leo kuna tofauti baina ya hadhi, lakini wakati utawadia ambapo hakutakuwepo na tofauti kama hizo: Hadhi ya wote hao ambao wamekuwa washindi itakuwa sawa, wote watakuwa wamehitimu kuwa wanadamu, na wataishi duniani kwa usawa, kwa maana kuwa wote watakuwa viumbe wenye sifa zinazostahili, na chochote watapewa kitakuwa sawa. Kwa kuwa nyakati za kazi ya Mungu ni tofauti, na madhumuni ya kazi yake ni tofauti pia, kama kazi hii inafanyika ndani yenu, nyinyi mnafaa kufanywa kamili na kuwa washindi; kama ingefanyika ng'ambo, basi wangukuwa na stahiki ya kuwa kundi la watu la kwanza kushindwa, na kundi la watu la kwanza la kufanywa kamilifu. Leo, kazi hii haifanywi kule ng'ambo, na kwa hivyo hawastahiki kufanywa wakamilifu ama kuwa washindi, na haiwezekani wao kukuwa kundi la kwanza. Kwa kuwa nia ya kazi ya Mungu ni tofauti, enzi ya kazi ya Mungu ni tofauti, na upeo wake ni tofauti, hivyo kuna kundi la kwanza, yaani, kuna washindi, na pia vile vile kutakuwa na kundi la pili ambalo ni la kufanywa kamilifu. Punde tu kunapokuwa na kundi la kwanza lililokamilishwa, kutakuwa na kiolezo na mfano, na hivyo mbeleni kutakuwa na kundi la pili na la tatu la wale wanakamilishwa, lakini ahera wote watakuwa sawa, na hakutakuwa na uainishaji wa hadhi. Wote watakuwa tu wamefanywa wakamilifu katika nyakati tofauti, na hakutakuwa na tofauti katika hadhi. Wakati utakapofika kila mtu amefanywa wakamilifu, na kazi ya ulimwengu mzima imehitimishwa, hakutakuwa na kulinganisha kwa hadhi, na wote watakuwa wa hadhi sawa. Leo, kazi hii inafanywa kati yenu ili muweze kuwa washindi. Kama ingefanyika nchini Uingereza, basi Uingereza ingekuwa kundi la kwanza, kwa njia sawa na vile mtakavyokuwa kundi la kwanza. Ni kwamba tu mmebarikiwa hasa na neema kwa njia ambayo kazi inatekelezwa ndani mwenu leo, na kama kama kazi hii haingefanywa ndani yenu, basi mangukuwa kundi la pili, au la tatu, au la nne, au la tano. Hii ni kwa sababu tu ya utofauti katika utaratibu wa kazi; kundi la kwanza na kundi la pili haliashirii kuwa moja ni la juu au la chini kuliko lingine, inaashiria tu utaratibu ambao upo wa watu hawa kufanywa wakamilifu. Leo maneno haya yanawasiliwa kwenu, lakini mbona hamkuwa mmefahamishwa mapema? Kwa sababu, bila mchakato, watu huwa wanakaa kuenda kuzidi kiasi. Kwa mfano, wakati huo Yesu alisema kwamba: "Kama Nilivyoondoka, ndivyo

Nitakavyowasili.” Leo, wengi wamepumbazwa na maneno haya, na wanataka tu kuvaa mavazi meupe wakisubiri kuchukuliwa kwenda mbinguni. Kwa hivyo, kuna maneno mengi ambayo hayawezi kusemwa mapema mno; kama yangesemwa mapema mno, mwanadamu angeenda kuzidi kiasi. Kimo cha mwanadamu ni kidogo mno, na hana uwezo wa kuona kuanzia mwanzo hadi mwisho wa ukweli wa maneno haya.

Wakati mtu anafanikiwa kupata maisha ya ukweli ya mwanadamu duniani na vikosi vizima vya Shetani vimefungwa, mwanadamu ataishi kwa urahisi katika ardhi. Mambo hayatakuwa magumu kama yalivyo sasa: Mahusiano ya binadamu, mahusiano ya kijamii, mahusiano changamani ya kifamilia...., haya ni ya kusumbua, machungu mno! Maisha ya mwanadamu hapa ni duni! Punde tu mwanadamu anaposhindwa, moyo wake na akili yake vitabadilika: atakuwa na moyo unaomcha Mungu na moyo ambao unampenda Mungu. Punde tu wote walio ulimwenguni ambao wanatafuta upendo wa Mungu wanaposhindwa, ambayo ni kusema, punde tu Shetani anaposhindwa, na punde tu Shetani—nguvu zote za giza—zimekwisha fungwa, basi maisha ya mwanadamu duniani yatakuwa yasiyotaabishwa, na ataweza kuishi huru duniani. Kama maisha ya mwanadamu hayana mahusiano ya kimwili, na hayana changamani za mwili, basi itakuwa rahisi mno. Mahusiano ya kimwili ya mwanadamu ni changamani mno, na kwa mwanadamu kuwa na mambo kama hayo ni thibitisho kuwa yeye bado hajajikomboa kutoka kwa ushawishi wa Shetani. Kama ungekuwa na uhusiano sawa na kila mmoja wa ndugu na dada, kama ungekuwa na uhusiano sawa na kila mmoja wa wanafamilia wako, basi hungekuwa na wasiwasi, na hungekuwa na haja ya kuhofia kuhusu mtu yeyote. Hakuna kitakachoweza kuwa bora zaidi, na kwa njia hii mwanadamu atapunguziwa nusu ya mateso yake. Kuishi maisha ya kawaida ya binadamu duniani, mwanadamu atakuwa sawa na malaika; ingawa atakuwa bado na mwili, atakuwa sawa na malaika. Hii ni ahadi ya mwisho, ni ahadi ya mwisho ambayo mwanadamu amezawadiwa. Leo mwanadamu anapitia kuadibu na hukumu; Je, unafikiri matukio kama haya ya mwanadamu hayana maana? Je, kazi ya kuadibu na kuhukumu inaweza kufanywa bila sababu. Hapo awali ilisemekana kuwa kuadibu na kuhukumu mwanadamu ni kumweka katika shimo lisilo na mwisho, ambayo ina maana ya kuchukua majaliwa na matarajio. Hii ni kwa ajili ya jambo moja: utakasaji wa mwanadamu. Mwanadamu hawekwi kwenye shimo lisilo na mwisho kimakusudi, ambapo baadaye Mungu hukata tamaa juu yake. Badala yake, ni ili kushughulika na uasi ndani ya mwanadamu, ili hatimaye mambo ndani ya mwanadamu yaweze kutakasika, ili aweze kuwa na ufahamu wa kweli wa Mungu, na awe kama mtu mtakatifu. Iwapo hii itafanywa, basi yote yatakuwa yametimia. Kwa kweli, wakati mambo hayo ndani ya mwanadamu ambayo yanapaswa kushughulikiwa yameshughulikiwa, na mwanadamu anakuwa na ushuhuda wa mwangwi, Shetani pia atashindwa, na hata ingawa kunaweza kuwa na mambo machache ambayo awali ndani ya mwanadamu hayakuwa yametakasika kabisa, punde tu Shetani

ameshindwa, Shetani hawezi tena kusababisha taabu, na wakati huo mwanadamu atakuwa ametakaswa kabisa. Mwanadamu hajawahi kupitia maisha kama haya, lakini wakati Shetani anashindwa, yote yatakuwa yametulizwa na mambo hayo pumbavu ndani ya mwanadamu yatatatuliwa yote; matatizo mengine yote yataisha punde tu tatizo kuu litakapokuwa limetatuliwa. Wakati wa kupata kwa mwili kwa Mungu duniani, wakati Yeye binafsi anafanya kazi miongoni mwa watu, kazi yote ambayo Yeye hufanya ni kwa ajili ya kumshinda Shetani, na Yeye atamshinda Shetani kupitia kumshinda mwanadamu na kuwafanya kamili. Wakati nyinyi mtakuwa na ushuhuda wa ajabu, hii, pia, itaonyesha kushindwa kwa Shetani. Kwanza mwanadamu anashindwa na hatimaye anafanywa kamili kabisa ili kumshinda Shetani. Kwa kiini, hata hivyo, pamoja na kushindwa kwa Shetani hii pia vilevile ni wokovu wa wanadamu wote kutoka kwa shimo la bahari hii ya mateso. Bila kujali kama kazi hii inatendeka katika ulimwengu mzima au katika nchi ya China, yote ni kwa ajili ya kumshinda Shetani na kuleta wokovu kwa wanadamu wote ili mwanadamu aweze kuingia pahali pa kupumzika. Mungu mwenye mwili, mwili huu wa kawaida, ni kwa usahihi kwa ajili ya kumshinda Shetani. Kazi ya Mungu mwenye mwili ni kuleta wokovu kwa wale wote walioko chini ya mbingu wanaompenda Mungu, ni kwa ajili ya kushinda wanadamu wote, na, zaidi ya hayo, kwa ajili ya kumshinda Shetani. Msingi wa kazi yote ya Mungu ya usimamizi haitengani na kushindwa kwa Shetani ili kuleta wokovu kwa watu wote. Kwa nini, katika mengi ya kazi hii, daima inasemekana kwenu kuwa na ushuhuda? Na ushuhuda huu unaelekezwa nani? Je, si unaelekezwa kwa Shetani? Ushuhuda huu unafanyiwa Mungu, na unafanywa ili kushuhudia kuwa kazi ya Mungu imetimiza matokeo yake. Kuwa na ushuhuda inahusiana na kazi ya kumshinda Shetani; kama hakungekuwa na vita dhidi ya Shetani, basi mwanadamu hangetakiwa kuwa na ushuhuda. Ni kwa sababu kwamba Shetani lazima ashindwe, kwa wakati huo huo kama kuokoa mwanadamu, Mungu anataka kwamba mwanadamu awe na ushuhuda wake mbele ya Shetani, ambao Yeye hutumia kufanya vita na Shetani. Kwa hivyo, mwanadamu ni mlengwa wa wokovu na chombo cha kumshinda Shetani, na kwa hivyo mwanadamu yumo katika msingi wa usimamizi mzima wa Mungu, na Shetani ni mlengwa wa uharibifu, adui. Unaweza kuhisi kuwa haujafanya kitu chochote, lakini kwa sababu ya mabadiliko katika tabia yako, umekuwa na ushuhuda, na ushuhuda huu unaelekezwa kwa Shetani na haufanywi kwa mwanadamu. Mwanadamu hajafaa ili afurahie ushuhuda kama huu. Je, jinsi gani yeye ataweza kuelewa kazi inayofanywa na Mungu? Mlengwa wa vita vya Mungu ni Shetani; mwanadamu, wakati huo huo, ni mlengwa wa wokovu. Mwanadamu ana tabia potovu ya kishetani, na hana uwezo wa kuelewa kazi hii. Hii ni kwa sababu ya kupotoshwa na Shetani and asili kwa mwanadamu, bali inaelekezwa na Shetani. Leo, kazi kuu ya Mungu ni kumshinda Shetani, yaani, kumshinda mwanadamu kabisa, ili kwamba mwanadamu awe na ushuhuda wa mwisho wa Mungu mbele ya Shetani. Kwa njia hii, mambo yote yatatimika. Kwa matukio mengi, kwa macho yako pekee inaonekana kwamba

hakuna chochote ambacho kimefanyika, lakini kwa kweli, kazi tayari imekamiliwa. Mwanadamu anahitaji kwamba kazi yote iliyokamiliwa iwe ya kuonekana, bali bila kuifanya inayoonekana wazi kwako, Nimemaliza kazi yangu, kwa kuwa Shetani ametii, ambayo ina maana kuwa yeye ameshindwa kabisa, ya kuwa busara yote ya Mungu, nguvu na mamlaka yamemshinda Shetani. Huu ndiyo ushuhuda mahsusi ambao ni lazima mtu awe nao, na ingawa haijidhihirishi kwa uwazi katika mwanadamu, ingawa haonekani kwa macho pekee, Shetani tayari ameshindwa. Ujumla wa kazi hii lazima uelekezwe dhidi ya Shetani, na inafanyika kwa ajili ya vita dhidi ya Shetani. Kwa hivyo, kuna mambo mengi ambayo mwanadamu haoni kuwa ni mafanikio, lakini ambayo, machoni pa Mungu, yalikuwa na mafanikio kwa muda mrefu uliopita. Hii ni moja ya ukweli wa ndani wa kazi yote ya Mungu.

Punde tu Shetani anaposhindwa, yaani, punde tu mwanadamu anaposhindwa kabisa, mwanadamu ataelewa kwamba kazi hii yote ni kwa ajili ya wokovu, na kuwa mbinu ya wokovu huu ni kurejesha kutoka kwa mikono ya Shetani. Miaka 6,000 ya kazi ya Mungu ya usimamizi imegawanywa katika hatua tatu: Enzi ya Sheria, Enzi ya Neema, na Enzi ya Ufalme. Hatua hizi zote tatu za kazi ni kwa ajili ya wokovu wa wanadamu, yaani, ni kwa ajili ya wokovu wa wanadamu ambao wamepotoshwa na Shetani kwa kiasi kikubwa. Wakati uo huo, hata hivyo, pia ni ili kwamba Mungu afanye vita na Shetani. Hivyo, kama kazi ya wokovu ilivyogawanywa katika hatua tatu, kwa hivyo pia vita dhidi ya Shetani vimegawanywa katika hatua tatu, na vipengele hivi viwili vya kazi ya Mungu vinafanywa sawia. Vita dhidi ya Shetani kwa kweli ni kwa ajili ya wokovu wa wanadamu, na kwa kuwa kazi ya wokovu wa wanadamu silo jambo linaloweza kukamilishwa kwa mafanikio katika hatua moja, vita dhidi ya Shetani pia vimegawanywa katika hatua na vipindi, na vita vinapiganwa dhidi ya Shetani kulingana na mahitaji ya mwanadamu na kiwango cha kupotoshwa kwa mwanadamu na Shetani. Pengine, katika mawazo ya mwanadamu, anaamini kuwa katika vita hivi Mungu atajiandaa kupigana na Shetani, katika njia sawa na vile ambavyo majeshi mawili yangepigana. Hili tu ni jambo ambalo akili ya mwanadamu ina uwezo wa kukisia, na ni wazo lisilo dhahiri kupita kiasi na lisiloweza kutendeka, na bado ndilo mwanadamu analiamini. Na kwa sababu Nasema hapa kuwa njia ya wokovu wa mwanadamu ni kupitia vita na Shetani, mwanadamu anawaza ya kwamba hivi ndivyo vita vinavyoendesha. Katika kazi ya wokovu wa mwanadamu, hatua tatu zimefanywa, ambayo ni kusema kuwa vita na Shetani vimegawanyika katika hatua tatu kabla ya kushindwa kabisa kwa Shetani. Na bado ukweli wa ndani wa kazi yote ya vita dhidi ya Shetani ni kwamba matokeo yake yanatimizwa kupitia kwa hatua kadhaa za kazi: kumpa mwanadamu neema, na kuwa sadaka ya dhambi ya mwanadamu, kuzisamehe dhambi za mwanadamu, kumshinda mwanadamu, na kumfanya mwanadamu akamilishwe. Kusema ukweli, vita na Shetani hajiandai kupigana na Shetani, bali ni wokovu wa mwanadamu, kuyashughulikia maisha ya mwanadamu,

na kubadilishwa kwa tabia ya mwanadamu ili kwamba aweze kumshuhudia Mungu. Hivi ndivyo Shetani anashindwa. Shetani anashindwa kwa kubadilisha tabia potovu ya mwanadamu. Wakati Shetani ameshindwa, yaani, wakati mwanadamu ameokolewa kabisa, basi Shetani aliyeaibika atafungwa kabisa, na kwa njia hii, mwanadamu atakuwa ameokolewa kabisa. Na kwa hivyo, kiini cha wokovu wa mwanadamu ni vita dhidi ya Shetani, na vita na Shetani vitajitokeza kimsingi katika wokovu wa mwanadamu. Hatua ya siku za mwisho, ambapo mwanadamu atashindwa, ni hatua ya mwisho katika vita dhidi ya Shetani, na pia kazi ya wokovu kamili wa mwanadamu kutoka kwa miliki ya Shetani. Maana ya ndani ya ushindi wa mwanadamu ni kurudi kwa mfano halisi wa Shetani, mtu ambaye amepotoshwa na Shetani, kwa Muumba baada ya ushindi wake, kwa njia ambayo atamwacha Shetani na kurejea kabisa kwa Mungu. Kwa njia hii, mwanadamu atakuwa ameokolewa kabisa. Na kwa hivyo, kazi ya ushindi ni kazi ya mwisho katika vita dhidi ya Shetani, na hatua ya mwisho katika kazi ya Mungu ya usimamizi kwa ajili ya kushindwa kwa Shetani. Bila kazi hii, wokovu kamili wa mwanadamu hatimaye haungewezekana, kushindwa kikamilifu kwa Shetani kusingewezekana, na mwanadamu kamwe hawangekuwa na uwezo wa kuingia kwenye hatima ya ajabu, ama kuwa huru kutoka kwa ushawishi wa Shetani. Kwa hivyo, kazi ya wokovu wa mwanadamu haiwezi kukamilishwa kabla vita dhidi ya Shetani havijahitimishwa, kwa kuwa msingi wa kazi ya Mungu ya usimamizi ni kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Mwanadamu wa kwanza kabisa alikuwa kwa mikono ya Mungu, lakini kwa sababu ya majaribu ya Shetani na upotovu wake, mwanadamu alifungwa na Shetani na kuanguka katika mikono ya yule mwovu. Kwa hivyo, Shetani akakuwa mlengwa wa kushindwa katika kazi ya Mungu ya usimamizi. Kwa sababu Shetani alichukua umiliki wa mwanadamu, na kwa sababu mwanadamu ndiye kiini cha usimamizi wote wa Mungu, kama mwanadamu ni wa kuokolewa, basi ni lazima anyakuliwe kutoka mikononi mwa Shetani, yaani mwanadamu ni lazima achukuliwe baada ya kutekwa nyara na Shetani. Hivyo, Shetani lazima ashindwe kupitia mabadiliko ya tabia ya mwanadamu ya zamani, mabadiliko ambayo hurejesha hisia zake za awali, na kwa njia hii, mwanadamu, ambaye ametekwa nyara, anaweza kunyakuliwa kutoka mikononi mwa Shetani. Kama mwanadamu anawekwa huru kutokana na ushawishi wa Shetani na utumwa wake, Shetani ataaibika, mwanadamu hatimaye atarejeshwa, na Shetani atakuwa ameshindwa. Na kwa sababu mwanadamu amewekwa huru kutoka kwa ushawishi wa giza wa Shetani, mwanadamu atakuwa mabaki ya vita hivi vyote, na Shetani atakuwa ndiye mlengwa ambaye ataadhibiwa punde tu vita hivi vitakapokamilika, na baada ya hapo kazi nzima ya wokovu wa mwanadamu itakuwa imekamilika.

Mungu hana nia mbaya kwa viumbe na anataka tu kumshinda Shetani. Kazi yote Yake—iwe ni kuadibu ama hukumu—inaelekezwa kwa Shetani; inafanyika kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu, yote ni kwa ajili ya kumshinda Shetani, na ina lengo moja: kufanya vita na Shetani

mpaka mwisho kabisa! Na Mungu kamwe hatapumzika kabla ya kuwa mshindi dhidi ya Shetani! Atapumzika tu punde atakapomshinda Shetani. Kwa sababu kazi yote ambayo inafanywa na Mungu inaelekezwa kwa Shetani, na kwa sababu wale waliopotoshwa na Shetani wote wanadhibitiwa na milki ya Shetani na wote wanamilikiwa na Shetani, bila kupigana dhidi ya Shetani na kuwa huru dhidi yake, Shetani hangepumzisha kushika kwake kwa watu hawa, na hawangeweza kupatwa. Kama hawangepatwa, ingethibitisha kwamba Shetani hajashindwa, ya kwamba hajatiishwa. Na kwa hivyo, katika miaka 6,000 ya mpango wa usimamizi wa Mungu, katika hatua ya kwanza Yeye alifanya kazi ya sheria, wakati wa hatua ya pili Yeye alifanya kazi ya Enzi ya Neema, yaani, kazi ya kusulubiwa, na wakati wa hatua ya tatu Yeye alifanya kazi ya kumshinda mwanadamu. Kazi hizi zote zinaelekezwa kwa kiwango ambacho Shetani alikuwa amewapotosha wanadamu, yote ni kwa ajili ya kumshinda Shetani, na hakuna hatua hata moja ambayo si kwa ajili ya kumshinda Shetani. Kiini cha miaka 6,000 ya kazi ya Mungu ya usimamizi ni vita dhidi ya joka kubwa jekundu, na kazi ya kusimamia watu pia ni kazi ya kumshinda Shetani, na kazi ya kufanya vita na Shetani. Mungu amepigana vita kwa miaka 6,000, na hivyo kufanya kazi kwa miaka 6,000, ili hatimaye kuleta mwanadamu katika ulimwengu mpya. Wakati Shetani atashindwa, mwanadamu atakuwa amewekwa huru kabisa. Je, huu si mwelekeo wa kazi ya Mungu hivi leo? Huu kwa hakika ni mwelekeo wa kazi ya leo: ukombozi kamili na kuwekwa huru kwa mwanadamu, ili kwamba asiwe chini ya sheria yoyote, wala asiwekewe mipaka na vifungu au vikwazo vyovyote. Kazi hii yote inafanywa kwa mujibu wa kimo chenu na kwa mujibu wa mahitaji yenu, kwa maana kuwa nyinyi mnapewa chochote mnachoweza kutimiza. Siyo namna ya “kumpeleka bata kwenye kitulio cha ndege,” ya kuwalazimishia chochote; badala yake, kazi hii yote inafanywa kwa mujibu wa mahitaji yenu ya kweli. Kila hatua ya kazi ni kwa mujibu wa mahitaji halisi na matakwa ya mwanadamu, na ni kwa ajili ya kumshinda Shetani. Kwa kweli, hapo mwanzo hapakuwa na vikwazo kati ya Muumba na viumbe Vyake. Vyote vinasababishwa na Shetani. Mwanadamu amegeuka asiyeweza kuona au kugusa chochote kwa sababu ya usumbufu wa Shetani na upotovu wake. Mwanadamu ndiye mwathiriwa, yule ambaye amedanganywa. Punde tu Shetani anaposhindwa, viumbe watamtazama Muumba, na Muumba ataangalia viumbe na kuweza kuwaongoza binafsi. Haya ndiyo tu maisha ambayo mwanadamu anapaswa kuwa nayo duniani. Na kwa hivyo, kazi ya Mungu kimsingi ni kwa ajili ya kumshinda Shetani, na punde tu Shetani anaposhindwa, mambo yote yatakuwa yametatuliwa. Leo, umeona kwamba kweli ni jambo kuu kwa Mungu kuja miongoni mwa wanadamu. Yeye hajakuja kutumia kila siku akitafuta makosa kwenu, kusema hivi au vile, au kuwawezesha tu kuona vile Yeye anavyofanana, na vile ambavyo Yeye huongea na kuishi. Mungu hajapata mwili ili kuwaruhusu mmtazamie Yeye tu, au kufungua macho yenu, ama kuwaruhusu kusikia mafumbo ambayo amenena kuhusu na mihuri saba ambayo amefungua. Badala yake, amepata mwili ili amshinde Shetani. Yeye binafsi amekuja miongoni mwa watu

katika mwili ili amwokoe mwanadamu, kufanya vita na Shetani, na huu ndio umuhimu wa Yeye kupata mwili. Kama haingekuwa ni kwa ajili ya kumshinda Shetani, basi asingefanya kazi hii binafsi. Mungu amekuja duniani kufanya kazi Yake miongoni mwa watu, kujifichua Mwenyewe kwa mwanadamu na kumruhusu mwanadamu kumtazamia; je, hili ni jambo dogo? Kwa kweli ni kuu! Si kama jinsi mwanadamu anavyofikiria kwamba Mungu amekuja ili mwanadamu aweze kumtazamia, ili mwanadamu aweze kuelewa kwamba Mungu ni wa ukweli na wala si yule asiye yakini ama mtupu, na ya kuwa Mungu ni wa fahari lakini pia mnyenyekevu. Je, inawezekana kuwa rahisi hivyo? Ni hasa kwa sababu Shetani amepotosha mwili wa mwanadamu, na mwanadamu ndiye Mungu anakusudia kuokoa, ya kuwa Mungu ni sharti achukue mwili ili afanye vita na Shetani na amchunge mwanadamu binafsi. Hii pekee ndiyo yenye manufaa kwa kazi Yake. Miili hiyo miwili ya Mungu ya nyama imekuwepo ili kumshinda Shetani, na pia imekuwepo ili imuokoe mwanadamu kwa njia bora zaidi. Hilo ni kwa sababu yule anayefanya vita na Shetani anaweza tu kuwa Mungu, awe ni Roho wa Mungu au ni mwili wenye nyama wa Mungu. Kwa kifupi, yule anayefanya vita na Shetani hawezi kuwa ni malaika, sembuse kuwa mwanadamu, ambaye amepotoshwa na Shetani. Malaika hawana uwezo wa kuifanya, na mwanadamu ni dhaifu hata zaidi. Kwa hivyo, ikiwa Mungu anataka kufanyia kazi maisha ya mwanadamu, kama Yeye anataka kuja duniani binafsi kumwokoa mwanadamu, basi ni lazima Yeye binafsi apate mwili—yaani, lazima Yeye binafsi achukue mwili, na kwa utambulisho Wake wa asili na kazi ambayo ni lazima afanye, aje miongoni mwa wanadamu na kumwokoa mwanadamu binafsi. La sivyo, kama ingekuwa ni Roho wa Mungu au mwanadamu ndiye aliyefanya kazi hii, basi vita hivi daima vingeshindwa kutimiza matokeo yake, na kamwe havingekwisha. Wakati tu Mungu anapata mwili ili Yeye binafsi aende kwa vita dhidi ya Shetani miongoni mwa watu ndipo mwanadamu anapata nafasi ya wokovu. Aidha, hapo tu ndipo Shetani anaibishwa, na kuwachwa bila nafasi zozote za kutumia au mipango yoyote ya kutekeleza. Kazi inayofanywa na Mungu aliyepata mwili haiwezi kutimizwa na Roho wa Mungu, na hata zaidi haiwezi kufanywa na mtu yeyote mwenye mwili kwa niaba ya Mungu, kwa kuwa kazi ambayo Yeye hufanya ni kwa ajili ya maisha ya mwanadamu, na ili kubadilisha tabia potovu ya mwanadamu. Kama mwanadamu angeshiriki katika vita hivi, yeye angekimbia tu kwa vurugu ya huzuni, na hangekuwa na uwezo kabisa wa kubadilisha tabia potovu ya mwanadamu. Angekuwa hana uwezo wa kumwokoa mwanadamu kutoka msalabani, ama wa kushinda wanadamu wote waasi, lakini angeweza tu kufanya kazi kidogo ya zamani ambayo haiendi zaidi ya kanuni, au vinginevyo kazi ambayo haihusiani na kushindwa kwa Shetani. Kwa hivyo, mbona ujisumbue? Kuna umuhimu gani wa kazi ambayo haiwezi kuwapata wanadamu, sembuse kumshinda Shetani? Na kwa hivyo, vita dhidi ya Shetani vinaweza kufanywa tu na Mungu Mwenyewe, na itakuwa tu vigumu kwa mwanadamu kupigana vita hivyo. Wajibu wa mwanadamu ni kutii na kufuata, kwa kuwa mwanadamu hana uwezo wa kufanya kazi kama vile kuumba mbingu na

dunia, wala, zaidi ya hayo, hawezi kutekeleza kazi ya kupigana na Shetani. Mwanadamu anaweza tu kumtosheleza Muumba chini ya uongozi wa Mungu Mwenyewe, ambapo Shetani hushindiwa; hili ndilo jambo pekee ambalo mwanadamu anaweza kulitenda. Na kwa hivyo, kila wakati vita vipya vinapoanza, kila wakati kazi ya enzi mpya inapoanza, kazi hii inafanywa na Mungu binafsi, ambapo kupitia kazi hiyo Yeye huongoza enzi nzima, na kufungua njia mpya kwa ajili ya wanadamu wote. Pambazuko la kila enzi mpya ni mwanzo mpya katika vita na Shetani, ambapo kupitia hiyo mwanadamu anaingia akiwa mpya zaidi, ulimwengu wa kupendeza zaidi na enzi mpya ambayo inaongozwa na Mungu Mwenyewe. Mwanadamu ni bwana wa vitu vyote, lakini wote ambao wamepatwa watakuwa matunda ya vita dhidi ya Shetani. Shetani ndiye mpotoshaji wa vitu vyote, na ndiye mshindwa katika mwisho wa vita vyote, na pia ndiye atakayeadhibiwa kufuatia vita hivi. Miongoni mwa Mungu, mwanadamu na Shetani, ni Shetani pekee ndiye atachukiwa na kukataliwa. Wale waliopatwa na Shetani lakini hawarejeshwi na Mungu, wakati huo huo, watakuwa wale ambao watapokea adhabu kwa niaba ya Shetani. Kati ya hawa watatu, Mungu pekee ndiye anapaswa kuabudiwa na vitu vyote. Wale waliopotoshwa na Shetani lakini wanarejeshwa na Mungu na wale wanaofuata njia ya Mungu, wakati huo huo, wanakuwa wale ambao watapokea ahadi ya Mungu na kuhukumu wale waovu kwa niaba ya Mungu. Bila shaka Mungu atakuwa mshindi na Shetani bila shaka atashindwa, lakini miongoni mwa wanadamu kuna wale watakaoshinda na wale watakaoshindwa. Wale ambao watashinda ni wa washindi, na wale ambao watashindwa ni wale wa washindwa; huu ni uainishaji wa kila mmoja kufuatana na aina, na ni hitimisho la mwisho la kazi yote ya Mungu. Pia ni lengo la kazi yote ya Mungu, na kamwe haitabadilika. Msingi wa kazi kuu wa mpango wa usimamizi wa Mungu unalenga wokovu wa mwanadamu, na Mungu anakuwa mwili kimsingi kwa ajili ya msingi huu, kwa ajili ya kazi hii, na ili kumshinda Shetani. Mara ya kwanza Mungu kuwa mwili ilikuwa ili kumshinda Shetani: Yeye binafsi akawa mwili, na akasulubiwa msalabani binafsi, ili kukamilisha kazi ya vita vya kwanza, ambayo ilikuwa kazi ya ukombozi wa mwanadamu. Aidha, awamu hii ya kazi ilifanywa na Mungu binafsi, ambaye amekuwa mwili ili kufanya kazi yake miongoni mwa wanadamu, ili kusema neno lake binafsi na kumwezesha mwanadamu kumwona. Bila shaka, ni hakika kwamba Yeye hufanya kazi nyingine njiani, lakini sababu kuu ya kufanya kazi yake binafsi ni ili kumshinda Shetani, kushinda wanadamu wote, na kuwapata hawa watu. Na kwa hivyo, kazi ya Mungu kuwa na mwili ni jambo kuu kweli. Kama kusudi lake lilikuwa tu kumwonyesha mwanadamu kuwa Mungu ni mnyenyekevu na aliyefichika, na kuwa Mungu ni wa ukweli, kama ingelikuwa ni kwa ajili ya kufanya kazi hii, basi hakungekuwa na haja ya kuwa mwili. Hata kama Mungu hakuwa mwili, yeye angefichua unyenyekevu na usiri wake, ukuu wake na utakatifu, kwa mwanadamu moja kwa moja, lakini mambo kama hayo hayana uhusiano wowote na usimamizi wa mwanadamu. Mambo kama hayo hayana uwezo wa kumwoko mwanadamu au kumfanya awe kamili, na hata hayawezi kumshinda Shetani. Kama kushindwa

kwa Shetani kungehusisha Roho tu akipigana vita dhidi ya roho, basi kazi kama hii ingekuwa na thamani ndogo ya ukweli; haingeweza kumpata mwanadamu na ingeharibu hatima na matarajio ya mwanadamu. Kwa hivyo, kazi ya Mungu leo ni moja ambayo ina umuhimu kupindukia. Sio hivyo ili kwamba mwanadamu aweze kumwona, au ili macho ya mwanadamu yaweze kufunguliwa, au ili ampe msukumo kiasi na kutiwa moyo; kazi kama hii haina umuhimu. Kama unaweza tu kuongea kwa hekima ya sampuli hii, basi inathibitisha kuwa wewe haujui umuhimu wa ukweli wa Mungu kupata mwili.

Kazi mzima ya mpangilio wa usimamizi wa Mungu inafanywa binafsi na Mungu mwenyewe. Awamu ya kwanza—uumbaji wa ulimwengu—ilifanywa binafsi na Mungu Mwenyewe, na kama haikuwa hivyo, basi hakuna yeyote ambaye angekuwa na uwezo wa kumuumba mwanadamu; awamu ya pili ilikuwa ukombozi wa wanadamu wote, na pia ilifanywa binafsi na Mungu Mwenyewe, awamu ya tatu inaenda bila kusemwa: Kuna haja kuu zaidi ya mwisho wa kazi ya Mungu kufanywa na Mungu Mwenyewe. Kazi ya ukombozi, ushindi, kumpata, na kumkamilisha wanadamu wote inafanywa binafsi na Mungu Mwenyewe. Kama hangefanya kazi hii Yeye binafsi, basi utambulisho wake hauwezi kuwakilishwa na mwanadamu, au kazi kufanywa na mwanadamu. Ili kumshinda Shetani, ili kumpata mwanadamu, na ili kumpa mwanadamu maisha ya kawaida duniani, Yeye binafsi humwongoza mwanadamu na hufanya kazi binafsi miongoni mwa wanadamu; kwa ajili ya mpangilio mzima wa usimamizi, na kwa kazi yake yote, ni lazima Yeye binafsi afanye kazi hii. Kama mwanadamu anaamini tu kuwa Mungu alikuja kuonekana naye na kumfurahisha, basi imani kama hizo hazina thamani, na hazina umuhimu. Maarifa ya mwanadamu ni ya kijuujuu mno! Ni kwa Mungu kutekeleza kazi Yeye mwenyewe ndivyo Mungu anaweza kufanya kazi yake vizuri na kikamilifu. Mwanadamu hana uwezo wa kuifanya kwa niaba ya Mungu. Kwa kuwa yeye hana utambulisho wa Mungu ama kiini Chake, hana uwezo wa kufanya kazi hii, na hata kama mwanadamu angekuwa na uwezo, haingekuwa na matokeo yoyote. Wakati wa kwanza Mungu kuwa mwili kwa ajili ya ukombozi, ilikuwa ni ili kuwakomboa wanadamu wote kutoka kwa dhambi, ili kufanya mwanadamu aweze kutakaswa na kusamehewa dhambi zake. Kazi ya ushindi pia inafanywa na Mungu binafsi miongoni mwa wanadamu. Kama, katika awamu hii, Mungu angekuwa wa kusema tu ya unabii, basi nabii au mtu ambaye ana kipawa angepatikana wa kuchukua nafasi Yake; kama unabii pekee ungesemwa, mwanadamu angechukua nafasi ya Mungu. Lakini ikiwa mwanadamu binafsi angefanya kazi ya Mungu Mwenyewe na angefanya kazi kwa maisha ya mwanadamu, haingewezekana kwake kufanya kazi hii. Ni lazima ifanywe na Mungu Mwenyewe binafsi: Ni lazima Mungu binafsi awe mwili ili kufanya kazi hii. Katika Enzi ya Neno, kama unabii pekee ungesemwa, basi Isaya au nabii Eliya wangepatikana wakifanya kazi hii, na hakungekuwepo na haja ya Mungu Mwenyewe kuifanya kazi hii binafsi. Kwa sababu

kazi ambayo inafanywa katika awamu hii si tu ya kuongea kuhusu unabii, na kwa sababu ni ya umuhimu mkubwa zaidi kuwa kazi ya maneno inatumiwa kumshinda mwanadamu na kumshinda Shetani, kazi hii haiwezi fanywa na mwanadamu, na ni lazima ifanywe na Mungu Mwenyewe binafsi. Katika Enzi ya Sheria Yehova alifanya sehemu ya kazi ya Mungu, ambapo baadaye alinena baadhi ya maneno na kufanya baadhi ya kazi kupitia kwa manabii. Hiyo ni kwa sababu mwanadamu angemwakilisha Yehova katika kazi yake, na waonaji wangeweza kutabiri mambo na kutafsiri baadhi ya ndoto kwa niaba Yake. Kazi iliyofanyika hapo mwanzo haikuwa kazi ya kubadilisha tabia ya mwanadamu moja kwa moja, na ilikuwa bila uhusiano na dhambi ya mwanadamu, na mwanadamu alitakiwa tu atii sheria. Kwa hivyo, Yehova hakuwa wa kuwa na mwili na kujifichua Mwenyewe kwa mwanadamu; badala yake Yeye aliongea moja kwa moja na Musa na wengine, akawafanya wao kusema na kufanya kazi kwa niaba yake, na kusababisha wao wafanye kazi moja kwa moja miongoni mwa wanadamu. Awamu ya kwanza ya kazi ya Mungu ilikuwa uongozi wa mwanadamu. Ilikuwa ndio mwanzo wa vita dhidi ya Shetani, lakini vita hivi vilikuwa bado kuanza rasmi. Vita rasmi dhidi ya Shetani vilianza na kupata mwili kwa Mungu kwa mara ya kwanza, na vimeendelea hadi leo. Tukio la kwanza la vita hivi ni wakati Mungu aliyepata mwili alisulubishwa msalabani. Kusulubiwa kwa Mungu aliyekuwa mwili kulimshinda Shetani, na ilikuwa mafanikio ya awamu ya kwanza katika vita. Wakati Mungu mwenye mwili alianza kufanya kazi kwa mwanadamu moja kwa moja, huu ulikuwa mwanzo rasmi wa kazi ya kumrejesha mwanadamu, na kwa sababu hii ilikuwa kazi ya kubadilisha tabia ya zamani ya mwanadamu, ilikuwa kazi ya kufanya vita na Shetani. Awamu ya kazi iliyofanywa na Yehova hapo mwanzo ilikuwa tu ya uongozi wa maisha ya mwanadamu duniani. Ilikuwa ndio mwanzo wa kazi ya Mungu, na hata ingawa ilikuwa bado haijashirikisha vita vyovyote, au kazi kuu yeyote, ilikuwa imeweka msingi kwa ajili ya kazi ya vita vijavyo. Baadaye, awamu ya pili ya kazi wakati wa Enzi ya Neema ilihusisha kubadilisha tabia ya zamani ya mwanadamu, ambayo ina maana kuwa Mungu Mwenyewe alitengeneza kwa ustadi kazi ya mwanadamu. Hii ilikuwa ni lazima ifanywe na Mungu: ilihitaji kuwa Mungu binafsi awe mwili, na kama hangekuwa mwili, hakuna mwingine angeweza kuchukua nafasi yake katika awamu hii ya kazi, kwa kuwa iliwakilisha kazi ya kupambana dhidi ya Shetani moja kwa moja. Kama mtu angekuwa amefanya kazi hii kwa niaba ya Mungu, wakati mwanadamu alisimama mbele ya Shetani, Shetani hangeweza kutii na haingewezekana kumshinda yeye. Ilibidi iwe Mungu aliyepata mwili aliyekuja kumshinda, kwa kuwa kiini cha Mungu mwenye mwili bado ni Mungu, Yeye bado ni maisha ya mwanadamu, na bado Yeye ni Muumba; chochote kitakachotokea, utambulisho Wake na kiini havitabadilika. Na kwa hivyo, Yeye alivaa mwili na alifanya kazi ili kusababisha kujisalimisha kwa Shetani. Katika awamu ya kazi ya siku za mwisho, kama mwanadamu angefanya kazi hii na angefanywa kusema maneno moja kwa moja, basi hangeweza kusema maneno hayo, na kama unabii ungesemwa, basi haungekuwa na uwezo

wa kumshinda mwanadamu. Kwa kuchukua mwili, Mungu huja kumshinda Shetani na kusababisha kujisalimisha kwake kamili. Wakati Yeye atamshinda Shetani kabisa, kumshinda mwanadamu kikamilifu, na kumpata mwanadamu kabisa, awamu hii ya kazi itakamilika na mafanikio kutimizwa. Katika usimamizi wa Mungu, mwanadamu hawezi kuwa naibu wa Mungu na kuwa Mungu wakati hayupo. Hasa, kazi ya kuongoza enzi na kuzindua kazi mpya ina haja kubwa zaidi kufanywa binafsi na Mungu Mwenyewe. Kumpa mwanadamu ufunuo na kwa kumpa yeye unabii kunaweza kufanywa na mwanadamu, lakini kama ni kazi ambayo ni lazima ifanywe na Mungu binafsi, kazi ya vita kati ya Mungu Mwenyewe na Shetani, basi kazi hii haiwezi kufanywa na mwanadamu. Katika awamu ya kwanza, wakati hakukuwepo na vita dhidi ya Shetani, Yehova binafsi aliongoza wana wa Israeli kutumia unabii uliosemwa na manabii. Baadaye, awamu ya pili ya kazi ilikuwa vita na Shetani, na Mungu Mwenyewe binafsi akawa mwili, kuja katika mwili, ili kufanya kazi hii. Chochote ambacho kinahusisha vita na Shetani pia kinahusisha kupata mwili kwa Mungu, ambayo ina maana kuwa vita hivi haviwezi kufanywa na mwanadamu. Kama mwanadamu angekuwa wa kufanya vita, hangeweza kumshinda Shetani. Jinsi gani yeye angekuwa na nguvu ya kupambana dhidi ya Shetani wakati bado yumo chini ya utawala wake? Mwanadamu yumo katikati: Kama wewe utaegemea kuelekea kwa Shetani wewe ni wa Shetani, lakini wewe ukimridhisha Mungu wewe ni wa Mungu. Kama mwanadamu angeweza kuwa mbadala wake Mungu katika kazi ya vita hivi, je, yeye angekuwa na uwezo wa kufanya hivyo? Kama angekuwa na uwezo, je, hangeangamia kitambo sana? Je, yeye si angekuwa ameingia katika ulimwengu wa jahanamu muda mrefu uliopita? Na hivyo, mwanadamu hana uwezo wa kuchukua nafasi ya Mungu katika kazi yake, ambayo ni kusema kwamba mwanadamu hana kiini cha Mungu, na kama ungepambana na Shetani hangeweza kumshinda Shetani. Mwanadamu anaweza tu kufanya baadhi ya kazi; anaweza kushinda baadhi ya watu, lakini hawezi kuwa mbadala wa Mungu katika kazi ya Mungu Mwenyewe. Je, ni jinsi gani mwanadamu atafanya vita na Shetani? Shetani ataweza kukushika mateka kabla hata hujaanza. Ni wakati Mungu Mwenyewe hufanya vita dhidi ya Shetani na mwanadamu kufuata na kutii Mungu katika msingi huu tu ndipo mwanadamu anaweza kupatwa na Mungu na kutoroka kutokana na vifungo vya Shetani. Kile mwanadamu anaweza kufikia kwa hekima yake na uwezo wake mwenyewe ni kidogo sana; hana uwezo wa kufanya mwanadamu akamilike, kumwongoza mwanadamu, na, zaidi ya hayo, kumshinda Shetani. Akili na hekima ya mwanadamu haviwezi kuharibu miradi ya Shetani, hivyo je, ni jinsi gani mwanadamu awezavyo kufanya vita na Shetani?

Wale wote ambao wamo tayari kufanywa kamili wana nafasi ya kukamilishwa, kwa hivyo kila mtu ni sharti apumzike: katika siku zijazo ninyi wote mtaingia kwenye hatima. Lakini kama huko tayari kufanywa kamili, na huko tayari kuingia katika ufalme wa kustaajibisha, basi hilo ni

tatizo lako mwenyewe. Wale wote ambao wako tayari kufanywa kamili na ni waaminifu kwa Mungu, wale wote ambao hutii, na wale wote ambao hufanya kazi yao kwa uaminifu watu wote kama hawa wanaweza kufanywa kamili. Leo, wale wote ambao hawatekelezi majukumu yao kwa uaminifu, wale wote ambao si waaminifu kwa Mungu, wale wote ambao hawajiwasilishi kwa Mungu, hasa wale ambao wamepokea kupata nuru na mwangaza wa Roho Mtakatifu lakini hawawezi mafundisho hayo kwenye vitendo—watu wote kama hawa hawawezi kufanywa kamili. Wote wale ambao wako tayari kuwa waaminifu na kumtii Mungu wanaweza kufanywa kamili, hata kama ni wapumbavu kwa kiasi kidogo, wote hao ambao wako tayari kufuatilia wanaweza kufanywa kamili. Hakuna haja ya kuwa na wasiwasi kuhusu hili. Ili mradi umo tayari kufuata mwelekeo huu, unaweza kufanywa kamili. Mimi sina nia ya kuwacha au kuondoa chochote kati ya hizo miongoni mwenu, lakini ikiwa mwanadamu hajitahidi kufanya vyema, basi utakuwa unajiangamiza mwenyewe; siyo Mimi ndiye ninakuondoa, lakini ni wewe mwenyewe. Kama wewe mwenyewe hutajitahidi kufanya vyema—ikiwa wewe ni mvivu, au hutekelezi jukumu lako, au si mwaminifu, au hufuati ukweli na daima unafanya unavyotaka, ukitenda bila kujali, ukipigania umaarufu wako na bahati yako mwenyewe na huna maadili katika kushirikiana na jinsia tofauti, basi utabeba mzigo wa dhambi zako mwenyewe; hustahili huruma ya yeyote. Lengo langu ni kwa ajili ya nyinyi nyote mfanywe kamilifu, na kuwa angalao muweze kushindwa, ili awamu hii ya kazi iweze kumalizika kwa mafanikio. Mapenzi ya Mungu ni kuwa kila mtu aweze kufanywa kamili, na kupatwa naye hatimaye, na kutakaswa naye kabisa, na kuwa mmoja anayependwa na Yeye. Haijalishi kama Ninasema nyinyi ni wa fikra za kurudi nyuma au wa kimo cha umaskini—hii yote ni ukweli. Huku kusema kwangu hakuthibitishi kuwa Mimi nina nia kukuacha wewe, kwamba Mimi Nimepoteza matumaini kwenu, au kwa kiasi kidogo kwamba sina nia ya kuwaokoa. Leo Nimekuja kufanya kazi ya ukombozi wenu, ambayo ni kusema kuwa kazi ambayo Mimi hufanya ni mwendelezo wa kazi ya ukombozi. Kila mtu ana nafasi ya kufanywa kamili: Ili mradi uko tayari, ili mradi ufuate, na mwishowe wewe utaweza kutimiza matokeo haya, na hakuna hata mmoja wenu ambaye ataachwa. Kama wewe ni mtu wa kimo cha umasikini, mahitaji Yangu kwenu yatakuwa kwa mujibu wa kimo chako cha umaskini; kama wewe ni wa kimo cha juu, mahitaji Yangu kwako yatakuwa kwa mujibu wa kimo chako cha juu; kama wewe ni mjinga na hujui kusoma na kuandika, mahitaji Yangu kwako yatakuwa kwa mujibu wa ujinga wako; kama wewe unajua kusoma na kuandika, mahitaji Yangu kwako yatakuwa kwa mujibu wa ukweli kwamba wewe unajua kusoma na kuandika; kama wewe ni mkongwe, mahitaji Yangu kwako yatakuwa kwa mujibu wa umri wako; kama wewe una uwezo wa kutoa ukarimu, mahitaji Yangu kwako yatakuwa kwa mujibu wa hilo; kama wewe unasema huwezi kutoa ukarimu, na unaweza tu kufanya kazi fulani, iwe ni kueneza injili, au kuchunga huduma ya kanisa, au kuhudhuria mambo mengine kwa ujumla, Ukamilifu Wangu kwako utakuwa kwa mujibu wa kazi ambayo wewe hufanya. Kuwa mwaminifu, kutii hadi mwisho

kabisa, na kutafuta upendo mkuu wa Mungu—mambo haya ni lazima uyakamilishe, na hakuna vitendo vizuri zaidi kuliko mambo haya matatu. Hatimaye, mtu anatakiwa kuyafikia mambo haya matatu, na kama anaweza kuyafikia hayo atafanywa kamili. Lakini, zaidi ya yote, ni lazima ujitahidi na kuendelea kwa bidii, na usiwe wa kukaa tu kuelekea hapo. Nimesema kwamba kila mtu ana nafasi ya kufanywa mkamilifu, na ana uwezo wa kukamilishwa, na hili ni kweli, lakini hujaribu kuwa bora zaidi katika ufuatiliaji wako. Kama huwezi kuvifikia vigezo hivyo vitatu, mwishowe lazima uondolewe. Nataka kila mtu afaulu kufikia wengine, nataka kila mtu awe na kazi na kupata nuru wa Roho Mtakatifu, na kuwa na uwezo wa kutii hadi mwisho kabisa, kwa sababu huu ni wajibu wa kila mmoja wenu ambao mnapaswa kufanya. Wakati nyinyi wote mmetimiza wajibu wenu, mtakuwa wote mmefanywa kamili, mtakuwa pia na ushuhuda wa kustaajabisha. Wale wote walio na ushuhuda ni wale ambao wamekuwa na ushindi juu ya Shetani na wanapewa ahadi ya Mungu, na wao ndio watakaobaki kuishi katika hatima ya ajabu.

Mungu na Mwanadamu Wataingia Rahani Pamoja

Mwanzoni, Mungu alikuwa anapumzika. Hakukuwa na binadamu ama kitu chochote kingine duniani wakati huo, na Mungu hakuwa amefanya kazi yoyote ile. Mungu alianza tu kazi Yake ya usimamizi baada ya binadamu kuwepo na baada ya binadamu kupotoshwa. Kutoka hapa kuendelea, Mungu hakupumzika tena lakini badala yake Alianza kufanya kazi miongoni mwa binadamu. Ilikuwa kwa sababu ya upotovu wa binadamu ndipo Mungu alichukuliwa kutoka kwa pumziko Lake, na ilikuwa pia kwa sababu ya uasi wa malaika mkuu ndipo Mungu alichukuliwa kutoka kwa pumziko Lake. Iwapo Mungu hatamshinda Shetani na kuokoa binadamu, ambao wamepotoshwa, Mungu hatawahi tena kuweza kuingia rahani. Mungu anakosa pumziko akosavyo mwanadamu. Wakati Mungu ataingia rahani tena, mwanadamu pia ataingia rahani. Maisha ya pumziko ni yale bila vita, bila uchafu, bila udhalimu unaoendelea. Hii ni kusema kwamba hayana unyanyasaji wa Shetani (hapa “Shetani” inamaanisha nguvu za uhasama), upotovu wa Shetani, na pia uvamizi wa nguvu yoyote inayompinga Mungu. Kila kitu kinafuata aina yake na kuabudu Bwana wa uumbaji. Mbingu na dunia ni shwari kabisa. Haya ni maisha matulivu ya binadamu. Mungu aingiapo rahani, hakuna udhalimu wowote utakaoendelea duniani, na hakutakuwa na uvamizi wowote wa nguvu za uhasama. Binadamu pia wataingia ulimwengu mpya; hawatakuwa tena binadamu waliopotoshwa na Shetani, lakini badala yake binadamu ambao wameokolewa baada ya kupotoshwa na Shetani. Siku ya pumziko ya binadamu pia ni siku ya pumziko ya Mungu. Mungu alipoteza pumziko Lake kwa sababu wanadamu hawakuweza kuingia rahani; haikuwa kwamba Hakuweza awali kupumzika. Kuingia rahani hakumaanishi kwamba mambo yote yatakoma kusonga, ama kwamba mambo yote yatakoma kuendelea, wala hakumaanishi kwamba Mungu atakoma kufanya kazi ama mwanadamu atakoma kuishi. Ishara ya kuingia rahani ni kama hii: Shetani ameangamizwa; wale watu waovu

wanaomuunga mkono Shetani kwa kufanya maovu wameadhibiwa na kuondolewa; nguvu zote za uhasama kwa Mungu zimekoma kuwepo. Mungu kuingia rahani kunamaanisha kwamba Hatafanya tena kazi Yake ya wokovu wa binadamu. Binadamu kuingia rahani kunamaanisha kwamba binadamu wote wataishi ndani ya mwangaza wa Mungu na chini ya baraka Zake; hakutakuwa na upotovu wowote wa Shetani, wala maovu yoyote kutokea. Binadamu wataishi kama kawaida duniani, na wataishi chini ya ulinzi wa Mungu. Mungu na mwanadamu waingiapo rahani pamoja, kutamaanisha kwamba binadamu wameokolewa na kwamba Shetani ameangamizwa, kwamba kazi ya Mungu ndani ya mwanadamu imemalizika kabisa. Mungu hataendelea tena kufanya kazi ndani ya mwanadamu, na mwanadamu hataendelea tena kumilikiwa na Shetani. Kwa hivyo, Mungu hatakuwa shughulini tena, na mwanadamu hatakimbiakimbia tena; Mungu na mwanadamu wataingia rahani wakati huo huo. Mungu atarudia nafasi yake ya awali, na kila mtu atarudia nafasi yake husika. Hizi ndizo hatima ambazo Mungu na mwanadamu wataishi ndani kwa utaratibu huu baada ya mwisho wa usimamizi wote wa Mungu. Mungu ana hatima ya Mungu na mwanadamu ana hatima ya mwanadamu. Apumzikapo, Mungu ataendelea kuwaongoza binadamu wote kwa maisha yao duniani. Akiwa kwa mwangaza wa Mungu, mwanadamu atamwabudu Mungu wa kweli aliye mbinguni. Mungu hataishi tena miongoni mwa binadamu, na mwanadamu pia hataweza kuishi na Mungu katika hitimisho la Mungu. Mungu na mwanadamu hawawezi kuishi ndani ya ulimwengu sawa; badala yake, wote wawili wana njia zao binafsi za kuishi. Mungu ndiye anayeongoza binadamu wote, wakati binadamu wote ni matokeo ya kazi ya Mungu ya usimamizi. Ni binadamu wanaoongozwa; kuhusu kiini, binadamu si sawa na Mungu. Kuingia rahani kunamaanisha kurudi pahali pa awali pa mtu. Kwa hivyo, Mungu aingiapo rahani, kunamaanisha kwamba Mungu amerudi pahali Pake pa awali. Mungu hataishi tena duniani ama kushiriki kwa furaha na mateso ya binadamu wakati yupo miongoni mwa binadamu. Binadamu wanapoingia rahani, kunamaanisha kwamba mwanadamu amekuwa kiumbe halisi; binadamu watamwabudu Mungu wakiwa duniani na kuwa na maisha ya kawaida ya wanadamu. Watu hawatakuwa tena wasiomtii Mungu ama kumpinga Mungu; watarudia maisha asili ya Adamu na Hawa. Haya ndiyo maisha na hatima binafsi ya Mungu na binadamu baada ya kuingia rahani. Kushindwa kwa Shetani ni mwelekeo usioepukika katika vita kati ya Mungu na Shetani. Kwa njia hii, kuingia kwa Mungu rahani baada ya kukamilika kwa kazi Yake ya usimamizi na wokovu kamili wa mwanadamu na kuingia rahani pia kunakuwa mielekeo isiyoepukika. Pahali pa pumziko pa mwanadamu ni duniani, na pahali pa Mungu pa pumziko ni mbinguni. Wakati binadamu wanamwabudu Mungu katika pumziko, wataishi duniani, na wakati Mungu anaongoza sehemu iliyobaki ya binadamu katika pumziko, Atawaongoza kutoka mbinguni, sio kutoka duniani. Mungu bado atakuwa Roho, wakati mwanadamu bado atakuwa mwili. Mungu na mwanadamu wote wawili wana njia zao tofauti za kupumzika. Mungu anapopumzika, Atakuja na kujitokeza miongoni mwa

mwanadamu, mwanadamu anapopumzika, ataongozwa na Mungu kutembea mbinguni na pia kufurahia maisha mbinguni. Baada ya Mungu na mwanadamu kuingia rahani, Shetani hatakuweko tena, na kama Shetani, wale watu waovu pia hawatakuweko tena. Kabla ya Mungu na mwanadamu kuingia rahani, wale watu waovu waliomtesa Mungu wakati mmoja duniani na adui waliokuwa hawamtii duniani watakuwa tayari wameangamizwa; watakuwa wameangamizwa na majanga makubwa ya siku za mwisho. Baada ya hao watu waovu kuangamizwa kabisa, dunia haitajua tena unyanyasaji wa Shetani. Binadamu watapata wokovu kamili, na hapo tu ndipo kazi ya Mungu itaisha kabisa. Haya ndiyo masharti ya Mungu na mwanadamu kuingia rahani.

Kukaribia kwa mwisho wa kila kitu kunaonyesha mwisho wa kazi ya Mungu na kunaonyesha mwisho wa maendeleo ya binadamu. Hii inamaanisha kwamba binadamu kama walivyopotoshwa na Shetani wamefika mwisho wao wa maendeleo, na kwamba vizazi vya Adamu na Hawa vitakuwa vimekamilisha uenezi wake. Na pia inamaanisha ya kwamba itawezekana kwa binadamu kama hawa, baada ya kupotoshwa na Shetani, kuendelea kustawi. Adamu na Hawa wa mwanzoni hawakuwa wamepotoshwa, lakini Adamu na Hawa waliofukuzwa kutoka Bustani ya Edeni walivurugwa na Shetani. Wakati Mungu na mwanadamu wanaingia rahani pamoja, Adamu na Hawa—waliofukuzwa kutoka Bustani ya Edeni—na vizazi vyao hatimaye watafika mwisho; binadamu wa baadaye bado watakuwa na vizazi vya Adamu na Hawa, lakini hawatakuwa watu wanaomilikiwa na Shetani. Badala yake, watakuwa watu waliookolewa na kutakaswa. Hawa watakuwa binadamu ambao wamehukumikiwa na kuadibiwa, na walio watakatifu. Hawa watu hawatakuwa sawa na jamii ya binadamu kama ilivyokuwa awali; mtu anaweza kusema kwamba hao ni watu wa aina tofauti kabisa na Adamu na Hawa wa awali. Hawa watu watakuwa wamechaguliwa kutoka miongoni mwa wote waliopotoshwa na Shetani, na watakuwa ndio watu ambao hatimaye wamesimama imara wakati wa hukumu na kuadibu kwa Mungu, watakuwa kundi la mwisho la watu miongoni mwa wanadamu potovu. Kundi hili la watu ndilo tu litaweza kuingia katika raha ya mwisho pamoja na Mungu. Wanaoweza kusimama imara wakati wa kazi ya Mungu ya hukumu na kuadibu siku za mwisho—yaani, wakati wa kazi ya mwisho ya utakaso—watakuwa wale watakaoingia katika raha ya mwisho na Mungu; kwa hivyo, wanaoingia rahani wote watakuwa wametoka katika ushawishi wa shetani na kupokewa na Mungu baada tu ya kupitia kazi Yake ya mwisho ya utakaso. Hawa watu ambao hatimaye wamepokewa na Mungu wataingia katika raha ya mwisho. Kiini cha kazi ya Mungu ya kuadibu na hukumu ni kutakasa binadamu, na ni ya siku ya raha ya mwisho. Vinginevyo, binadamu wote hawataweza kufuata aina yao ama kuingia katika raha. Hii kazi ni njia ya pekee ya binadamu kuingia rahani. Kazi ya Mungu ya utakaso pekee ndiyo itatakasa udhalimu wa binadamu, na kazi Yake ya kuadibu na hukumu pekee ndiyo itadhihirisha

hayo mambo yasiyotii miongoni mwa binadamu, hivyo kutenga wanaoweza kuokolewa kutoka wale wasioweza, na wale watakaobaki kutoka wale ambao hawatabaki. Kazi Yake itakapoisha, wale watu watakaoruhusiwa kubaki wote watatakaswa na kuingia katika hali ya juu zaidi ya ubinadamu ambapo watafurahia maisha ya pili ya binadamu ya ajabu zaidi duniani; kwa maneno mengine, wataingia katika siku ya binadamu ya raha na kuishi pamoja na Mungu. Baada ya wasioweza kubaki kupitia kuadibu na hukumu, umbo zao halisi zitafichuliwa kabisa; baada ya haya wote wataangamizwa na, kama Shetani, hawatakubaliwa tena kuishi duniani. Binadamu wa baadaye hawatakuwa tena na aina yoyote ya watu hawa; watu hawa hawafai kuingia eneo la raha ya mwisho, wala hawafai kuingia siku ya raha ambayo Mungu na mwanadamu watashiriki, kwani ni walengwa wa adhabu na ni waovu, na si watu wenye haki. Walikuwa wamekombolewa wakati mmoja, na pia walikuwa wamehukumiwa na kuadibiwa; walikuwa pia wamemhudumia Mungu wakati mmoja, lakini siku ya mwisho itakapofika, bado wataondolewa na kuangamizwa kwa sababu ya uovu wao na kwa sababu ya kutotii na kutokombolewa kwao. Hawatakuwa tena katika ulimwengu wa baadaye, na hawatakuweka tena miongoni mwa jamii ya binadamu ya baadaye. Watenda maovu wote na yeyote na wote ambao hawajaokolewa wataangamizwa wakati watakatifu miongoni mwa binadamu wataingia rahani, bila kujali kama wao ni roho za wafu ama wale wanaoishi bado katika mwili. Bila kujali enzi ya hizi roho zitendazo maovu na watu watenda maovu, ama roho za watu wenye haki na watu wanaofanya haki wako, mtenda maovu yeyote ataangamizwa, na yeyote mwenye haki ataishi. Iwapo mtu ama roho inapokea wokovu haiamuliwi kabisa kulingana na kazi ya enzi ya mwisho, lakini inaamuliwa kulingana na iwapo wamempinga ama kutomtii Mungu. Kama watu wa enzi ya awali walifanya maovu na hawangeweza kuokolewa, bila shaka wangukuwa walengwa wa adhabu. Kama watu wa enzi hii wanafanya maovu na hawawezi kuokolewa, hakika wao pia ni walengwa wa adhabu. Watu wanatengwa kwa msingi wa mema na mabaya, sio kwa msingi wa enzi. Baada ya kutengwa kwa msingi wa mema na mabaya, watu hawaadhibiwa ama kutuzwa mara moja; badala yake, Mungu atafanya tu kazi Yake ya kuwaadhibu waovu na kuwatuza wema baada ya Yeye kumaliza kutekeleza kazi Yake ya ushindi katika siku za mwisho. Kwa kweli, Amekuwa akitumia mema na mabaya kutenga binadamu tangu Afanye kazi Yake miongoni mwa binadamu. Atawatuza tu wenye haki na kuwaadhibu waovu baada ya kukamilika kwa kazi Yake, badala ya kuwatenga waovu na wenye haki baada ya kukamilika kwa kazi Yake mwishowe na kisha kufanya kazi Yake ya kuwaadhibu waovu na kuwatuza wazuri mara moja. Kazi Yake ya mwisho ya kuadhibu waovu na kuwatuza wazuri inafanywa kabisa ili kutakasa kabisa binadamu wote, ili Aweze kuleta binadamu watakatifu mno katika pumziko la milele. Hatua hii ya kazi Yake ni kazi Yake muhimu zaidi. Ni hatua ya mwisho ya kazi Yake yote ya usimamizi. Kama Mungu hangewaangamiza waovu lakini badala yake kuwaacha wabakie, basi binadamu wote bado hawangeweza kuingia rahani, na Mungu hawangeweza kuleta binadamu katika ulimwengu bora.

Kazi ya aina hii haingekuwa imekamili kabisa. Atakapomaliza kazi Yake, binadamu wote watakuwa watakatifu kabisa. Mungu anaweza kuishi kwa amani rahani kwa namna hii pekee.

Watu leo hawawezi kutengana na mambo ya mwili; hawawezi kuacha starehe za mwili, wala hawawezi kuiacha dunia, pesa, ama tabia yao potovu. Watu wengi wanaendelea na shughuli zao kwa hali ya uzembe. Kwa kweli, hawa watu hawana Mungu mioyoni mwao hata kidogo; zaidi ya hayo, hawamchi Mungu. Hawana Mungu mioyoni mwao, na hivyo hawawezi kutambua yote anayofanya Mungu, na hawawezi kabisa kuamini maneno Azungumzayo kwa mdomo Wake. Watu hawa ni wa mwili sana, wamepotoshwa sana na hawana ukweli wowote, zaidi ya hayo, hawaamini kwamba Mungu anaweza kuwa mwili. Yeyote asiyemwamini Mungu wa mwili—yaani, yeyote asiyeamini kazi na hotuba ya Mungu anayeonekana na haamini Mungu anayeonekana lakini badala yake anaabudu Mungu asiyeonekana mbinguni—hana Mungu katika moyo wake. Ni watu wasiomtii na wanaompinga Mungu. Watu hawa hawana ubinadamu na fahamu, kusema chochote kuhusu ukweli. Kwa watu hawa Mungu anayeonekana na kushikika hawezi kuaminika zaidi, lakini Mungu asiyeonekana wala kushikika ni Mungu wa kuaminika na pia Anayefurahisha nyoyo zao. Wanachotafuta si ukweli wa uhalisi, wala si kiini cha kweli cha uhai, wala nia za Mungu; badala yake, wanatafuta msisimko. Mambo yoyote yanayoweza kuwaruhusu kufikia tamaa zao ni, bila shaka, imani na shughuli zao. Wamwamini Mungu tu ili kuridhisha tamaa zao, si kutafuta ukweli. Hawa watu si watenda maovu? Wanajiamini sana, na hawaamini kwamba Mungu aliye mbinguni atawaangamiza, hawa “watu wazuri.” Badala yake, wanaamini kwamba Mungu atawaruhusu kubaki na, zaidi ya hayo, Atawatuza vizuri sana, kwani wamemfanyia Mungu mambo mengi na kuonyesha kiwango kikubwa cha “uaminifu” Kwake. Kama wangemtafuta Mungu anayeonekana, wangelipiza kisasi mara moja dhidi ya Mungu na kukasirika wakati hawatapata tamaa zao. Hawa ni watu waovu wanaotaka kuridhisha tamaa zao; si watu wa uadilifu wanaosaka ukweli. Watu kama hao ni wale wanaojulikana kama waovu wanaomfuata Kristo. Wale watu wasioutafuta ukweli hawawezi kuamini ukweli. Hawawezi kabisa kutambua matokeo ya baadaye ya binadamu, kwani hawaamini kazi ama hotuba yoyote ya Mungu anayeonekana, na hawawezi kuamini hitimisho la baadaye la binadamu. Hivyo, hata wakimfuata Mungu anayeonekana, bado wanatenda maovu na hawatafuti ukweli, wala hawatendi ukweli Ninaohitaji. Wale watu wasioamini kwamba wataangamizwa kinyume ni kwamba ni wale watu watakaoangamizwa. Wote wanajiamini kuwa wajanja sana, na wanaamini kwamba wao wenyewe ndio wanaotenda ukweli. Wanafikiria mwenendo wao mbovu kuwa ukweli na hivyo wanauthamini. Hawa watu waovu wanajiamini sana; wanachukua ukweli kuwa mafundisho ya dini, na kuchukua vitendo vyao vibovu kuwa ukweli, na mwishowe watavuna tu walichopanda. Watu wanapojiamini zaidi na wanapokuwa na kiburi zaidi, ndipo hawawezi zaidi kupata ukweli; watu wanapomwamini Mungu wa mbinguni zaidi, ndipo wanampinga Mungu

zaidi. Hawa ndio watu watakaoadhibiwa. Kabla ya binadamu kuingia rahani, iwapo kila aina ya mtu ataadhibiwa ama kutuzwa kutaamuliwa kulingana na iwapo wanatafuta ukweli, iwapo wanamjua Mungu, iwapo wanaweza kumtii Mungu anayeonekana. Waliomhudumia Mungu anayeonekana lakini bado hawamjui wala kumtii hawana ukweli. Watu hawa ni watenda maovu, na watenda maovu bila shaka wataadhibiwa; zaidi ya hapo, wataadhibiwa kulingana na mienendo yao mibovu. Mungu ni wa mwanadamu kumwamini, na pia Anastahili utii wa mwanadamu. Wale wanaomwamini tu Mungu asiye yakini na asiyeonekana ni wale wasiomwamini Mungu; zaidi ya hapo, hawawezi kumtii Mungu. Kama hawa watu bado hawawezi kumwamini Mungu anayeonekana wakati kazi Yake ya ushindi inakamilika, na pia wanaendelea kutomtii na kumpinga Mungu anayeonekana katika mwili, hawa wanaoamini isiyo yakini bila shaka, wataangamizwa. Ni kama ilivyo na wale miongoni mwenu—yeyote anayemtambua Mungu Aliyepata mwili kwa maneno lakini bado hatendi ukweli wa utii kwa Mungu Aliyepata mwili hatimaye ataondolewa na kuangamizwa, na yeyote anayemtambua Mungu anayeonekana na pia kula na kunywa ukweli ulioonyeshwa na Mungu anayeonekana lakini bado anamtafuta Mungu asiye yakini na asiyeonekana pia yeye ataangamizwa baadaye. Hakuna hata mmoja wa watu hawa anayeweza kubaki hadi wakati wa pumziko baada ya kazi ya Mungu kukamilika; hakuwezi kuwa yeyote kama watu hawa atakayebakia hadi wakati wa pumziko. Watu wenye pepo ni wale wasiotenda ukweli; asili yao ni ile inayompinga na kutomtii Mungu, na hawana nia hata kidogo za kumtii Mungu. Watu wote kama hao wataangamizwa. Iwapo una ukweli na iwapo unampinga Mungu hayo yanaamuliwa kulingana na asili yako, si kulingana na sura yako ama hotuba na mwenendo wako wa mara kwa mara. Asili ya kila mtu inaamua iwapo ataangamizwa; hii inaamuliwa kulingana na asili iliyofichuliwa na mienendo yao na kutafuta kwao ukweli. Miongoni mwa watu wanaofanya kazi sawa na pia kufanya kiasi sawa cha kazi, wale ambao asili yao ni nzuri na wanaomiliki ukweli ni watu wanaoweza kubaki, lakini wale ambao asili yao ya ubinadamu ni mbovu na wasiomtii Mungu anayeonekana ni wale watakaoangamizwa. Kazi ama maneno yoyote ya Mungu yanayoelekezwa kwa hatima ya binadamu yanahusiana na binadamu ipasavyo kulingana na asili ya kila mtu; hakuna kosa lolote litakalotokea, na hakutakuwa na kosa hata moja litakalofanywa. Ni pale tu ambapo watu wanafanya kazi ndipo hisia za binadamu ama maana itaingilia. Kazi anayofanya Mungu ndiyo inayofaa zaidi; hakika Hataleta madai ya uongo dhidi ya kiumbe yeyote. Sasa kuna watu wengi wasioweza kutambua hatima ya baadaye ya binadamu na ambao pia hawaamini maneno Nisemayo; wote wasioamini, pamoja na wasiotenda ukweli, ni mapepo!

Wanaotafuta na wasiotafuta sasa ni aina mbili tofauti ya watu, na wao ni aina mbili ya watu na hatima mbili tofauti. Wanaotafuta maarifa ya ukweli na kutenda ukweli ni watu ambao Mungu ataokoa. Wale wasiojua njia ya ukweli ni mapepo na adui; ni vizazi vya malaika mkuu na

wataangamizwa. Hata wacha Mungu wanaomwamini Mungu asiye yakini—je, si mapepo pia? Watu wanaomiliki dhamiri nzuri lakini hawakubali njia ya ukweli ni mapepo; asili yao ni ile inayompinga Mungu. Wale wasiokubali njia ya ukweli ni wale wanaompinga Mungu, na hata kama watu hawa wanavumilia taabu nyingi, bado wataangamizwa. Wasio tayari kuiwacha dunia, wasioweza kuvumilia kutengana na wazazi wao, wasioweza kuvumilia kujiondolea raha zao za mwili, wote hawamtii Mungu na wote wataangamizwa. Yeyote asiyemwamini Mungu aliyepata mwili ni pepo; zaidi ya hayo, wataangamizwa. Wanaoamini lakini hawatendi ukweli, wasiomwamini Mungu aliyepata mwili, na wale ambao hawaamini kabisa kuwepo kwa Mungu wataangamizwa. Yeyote anayeweza kubaki ni mtu ambaye amepitia uchungu wa usafishaji na kusimama imara; huyu ni mtu ambaye kweli amepitia majaribio. Yeyote asiyemtambua Mungu ni adui; yaani, yeyote aliye ndani ama nje ya mkondo huu ambaye hamtambui Mungu aliyepata mwili ni adui wa Kristo! Shetani ni nani, mapepo ni nani, na nani ni maadui wa Mungu kama si wapinzani wasiomwamini Mungu? Wao si watu wasiomtii Mungu? Wao si watu wanaodai kwa maneno kuamini lakini hawana ukweli? Wao si wale watu wanaofuata tu kupata kwa baraka lakini hawawezi kumshuhudia Mungu? Bado unachanganyika na wale mapepo leo na kuwa na dhamiri na mapenzi kwao, lakini kwa hali hii huenezi nia nzuri kuelekea kwa Shetani? Je, huchukuliwi kuwa unashiriki na mapepo? Kama watu siku hizi bado hawawezi kutofautisha kati ya mema na maovu, na wanaendelea kuwa wenye kupenda na kuhurumia bila kufikiri na bila nia yoyote ya kutafuta mapenzi ya Mungu au kuweza kwa njia yoyote kushikilia nia za Mungu kama zao wenyewe, basi miisho wao utakuwa dhalili zaidi. Yeyote asiyemwamini Mungu wa mwili ni adui wa Mungu. Kama unaweza kushikilia dhamiri na mapenzi kuelekea kwa adui, je, hujakosa hisia ya haki? Kama unalingana na wale Ninaowachukia na wale Nisiokubaliana nao, na bado unashikilia mapenzi na hisia za binafsi kwao, basi wewe si asiyetii? Humpingi Mungu kimakusudi? Je, mtu kama huyu anamiliki ukweli? Ikiwa watu wako na dhamiri kwa maadui, wana upendo kwa mapepo na wana huruma kwa Shetani, basi hawaikatizi kazi ya Mungu kimakusudi? Wale watu wanaomwamini Yesu tu na hawamwamini Mungu aliyepata mwili wakati wa siku za mwisho na wale wanaodai kwa maneno kumwamini Mungu aliyepata mwili lakini wanafanya maovu wote ni adui wa Kristo, sembuse wale watu wasiomwamini Mungu. Hawa watu wote wataangamizwa. Kiwango ambacho mwanadamu anamhukumu mwanadamu kinatokana na tabia zake; aliye na mwenendo mzuri ni mtu mwenye haki, na aliye na mwenendo wa kuchukiza ni mwovu. Kiwango ambacho Mungu anamhukumu mwanadamu kinatokana na iwapo asili ya mtu inamtii Yeye; anayemtii Mungu ni mtu mwenye haki, na asiyemtii Mungu ni adui na mtu mwovu, bila kujali iwapo tabia ya mtu huyu ni nzuri ama mbaya, na bila kujali iwapo hotuba ya mtu huyu ni sahihi ama si sahihi. Watu wengine wanatamani kutumia matendo mazuri kupata hatima nzuri ya baadaye, na watu wengine wanataka kutumia hotuba nzuri kununua hatima nzuri. Watu wanaamini kimakosa kwamba Mungu anaamua matokeo ya

mwanadamu kulingana na tabia ama hotuba yake, na kwa hivyo watu wengi watataka kutumia haya kupata fadhila ya muda mfupi kupitia udanganyifu. Watu ambao baadaye watasalimika kupitia pumziko wote watakuwa wamevumilia siku ya dhiki na pia kumshuhudia Mungu; wote watakuwa watu ambao wamefanya jukumu lao na wana nia ya kumtii Mungu. Wanaotaka tu kutumia fursa kufanya huduma ili kuepuka kutenda ukweli hawataweza kubaki. Mungu ana viwango sahihi vya mipangilio ya matokeo ya kila mtu; Hafanyi tu maamuzi haya kulingana na maneno na mwenendo wa mtu, wala Hayafanyi kulingana na tabia zao wakati wa kipindi kimoja cha muda. Hakika Hatakuwa na huruma na mwenendo wowote mbaya wa mtu kwa sababu ya huduma ya mtu ya zamani kwa Mungu, wala Hatamnusuru mtu kutokana na kifo kwa sababu ya gharama kwa Mungu ya mara moja. Hakuna anayeweza kuepuka adhabu ya uovu wake, na hakuna anayeweza kuficha tabia zake mbovu na hivyo kuepuka adhabu ya maangamizi. Kama mtu anaweza kweli kufanya jukumu lake, basi inamaanisha kwamba ni mwaminifu milele kwa Mungu na hatafuti tuzo, bila kujali iwapo anapokea baraka ama bahati mbaya. Kama watu wana uaminifu kwa Mungu waonapo baraka lakini wanapoteza uaminifu wao wasipoweza kuona baraka na mwishowe bado wasiweze kumshuhudia Mungu na bado wasiweze kufanya jukumu lao kama wapasavyo, hawa watu waliomhudumia Mungu wakati mmoja kwa uaminifu bado wataangamizwa. Kwa ufupi, watu waovu hawawezi kuishi milele, wala hawawezi kuingia rahani; watu wenye haki tu ndio mabwana wa pumziko. Baada ya binadamu kuingia katika njia sawa, watu watakuwa na maisha ya kawaida ya binadamu. Wote watafanya jukumu lao husika na kuwa waaminifu kabisa kwa Mungu. Watatoa kabisa kutotii kwao na tabia yao iliyopotoshwa, na wataishi kwa ajili ya Mungu na kwa sababu ya Mungu. Watakosa uasi na upinzani. Wataweza kabisa kumtii Mungu. Haya ndiyo maisha ya Mungu na mwanadamu na maisha ya ufalme, na ni maisha ya pumziko.

Wanaopeleka watoto na jamaa zao wasioamini kabisa kanisani ni wachoyo sana na wanaonyesha ukarimu wao. Watu hawa wanalenga tu kuwa wenye upendo, bila kujali iwapo wanaamini au la na iwapo ni mapenzi ya Mungu. Wengine wanaleta wake zao mbele ya Mungu, ama kuleta wazazi wao mbele ya Mungu, na bila kujali iwapo Roho Mtakatifu anakubali ama anafanya kazi Yake, kwa upofu “wanawachukua watu wenye vipaji” kwa ajili ya Mungu. Kuna faida gani inayoweza kupatikana kutokana na kueneza ukarimu huu kwa watu hawa wasioamini? Hata kama hawa wasioamini wasio na uwepo wa Roho Mtakatifu wanapambana kumfuata Mungu, bado hawawezi kuokolewa kama mtu anavyodhani wanaweza. Wanaopokea wokovu kwa kweli si rahisi hivyo kuwapata. Wale ambao hawajapitia kazi ya Roho Mtakatifu na majaribio na hawajakamilishwa na Mungu aliyepata mwili hawawezi kukamilika kabisa. Kwa hivyo, watu hawa hawana uwepo wa Roho Mtakatifu kutoka wakati wanaanza kumfuata Mungu kwa jina. Kulingana na hali yao halisi, hawawezi tu kufanywa kamili. Hivyo, Roho Mtakatifu

Haamui kutumia nguvu nyingi kwao, wala Hawapatii nuru yoyote ama kuwaongoza kwa njia yoyote; Anawaruhusu tu kufuata na hatimaye kufichua matokeo yao—haya yametosha. Shauku na nia za mwanadamu zinatoka kwa Shetani, na hakuna vile zinaweza kukamilisha kazi ya Roho Mtakatifu. Bila kujali mtu ni mtu wa aina gani, mtu lazima awe na kazi ya Roho Mtakatifu—je, mtu anaweza kumkamlisha mtu? Mbona mume anampenda mke wake? Na mbona mke anampenda mume wake? Mbona watoto ni watiifu kwa wazazi wao? Na mbona wazazi wanawapenda sana watoto wao? Watu kweli wana nia za aina gani? Je, si kuweza kukidhi mipango na tamaa zao za ubinafsi? Kweli ni ya mpango wa usimamizi wa Mungu? Ni ya kazi ya Mungu? Ni ya kutimiza wajibu wa kiumbe? Waliomwamini Mungu kwanza na hawangepata uwepo wa Roho Mtakatifu hawawezi kupata kazi ya Roho Mtakatifu; imeamuliwa kwamba watu hawa wataangamizwa. Bila kujali kiasi cha upendo ambao mtu anao kwao, hauwezi kuchukua nafasi ya kazi ya Roho Mtakatifu. Shauku na upendo wa mwanadamu unawakilisha nia za mwanadamu, lakini haviwezi kuwakilisha nia za Mungu na haviwezi kuchukua nafasi ya kazi ya Mungu. Hata mtu akieneza kiasi kikubwa zaidi cha upendo ama huruma kwa hao watu wanaomwamini Mungu kwa jina na kujifanya kumfuata Yeye lakini hawajui ni nini maana ya kumwamini Mungu, bado hawatapata huruma ya Mungu ama kupata kazi ya Roho Mtakatifu. Hata kama watu wanaomfuata Mungu kwa dhati ni wenye akili ndogo na hawawezi kuelewa kweli nyingi, bado wanaweza kupata kazi ya Roho Mtakatifu mara kwa mara, lakini wale walio wa akili nzuri kidogo, lakini hawaamini kwa dhati hawawezi kabisa kupata uwepo wa Roho Mtakatifu. Hakuna kabisa uwezekano wowote wa wokovu na watu hawa. Hata wakisoma maneno ya Mungu au wasikilize mahubiri mara kwa mara ama hata kumwambia Mungu sifa, mwishowe hawataweza kubaki mpaka wakati wa pumziko. Iwapo mtu anatafuta kwa dhati hakuamuliwi na jinsi wengine wanamhukumu ama jinsi wengine karibu wanamwona, lakini kunaamuliwa na iwapo Roho Mtakatifu anamfanyia kazi na iwapo ana uwepo wa Roho Mtakatifu, na kunaamuliwa zaidi na iwapo tabia yake inabadilika na iwapo ana maarifa ya Mungu baada ya kupitia kazi ya Roho Mtakatifu kwa muda fulani; ikiwa Roho Mtakatifu anamfanyia mtu kazi, tabia ya mtu huyu itabadilika polepole, na mtazamo wake wa kumwamini Mungu utakua safi polepole. Bila kujali muda gani mtu anamfuata Mungu, kama wamebadilika, hii inamaanisha kwamba Roho Mtakatifu anafanya kazi kwake. Kama hawajabadilika, inamaanisha kwamba Roho Mtakatifu hafanyi kazi kwake. Hata kama hawa watu wanatoa huduma fulani, wanachochewa na nia zao za kupata bahati nzuri. Huduma ya mara kwa mara haiwezi kuchukua nafasi ya mabadiliko katika tabia yao. Hatimaye, bado wataangamizwa, kwani hakuna haja ya wale wanaotoa Huduma ndani ya ufalme, wala hakuna haja ya yeyote ambaye tabia yake haijabadilika kuwahudumia wale watu ambao wamekamilishwa na walio waaminifu kwa Mungu. Hayo maneno kutoka zamani, “Wakati mtu anamwamini Bwana, bahati inatabasamu kwa familia yake nzima,” yanafaa kwa Enzi ya Neema lakini hayana uhusiano na

hatima ya mwanadamu. Yalifaa tu kwa hatua ya wakati wa Enzi ya Neema. Maana iliyokusudiwa ya maneno haya inaelekezwa kwa amani na baraka yakinifu ambazo watu wanafurahia; hayamaanishi kwamba familia nzima ya anayemwamini Bwana itaokolewa, wala hayamaanishi kwamba wakati mtu anapata bahati nzuri, familia yake nzima pia itaingia rahani. Iwapo mtu anapokea baraka ama kupata bahati mbaya inaamuliwa kulingana na kiini cha mtu, na haiamuliwi kulingana na asili ya kawaida ambayo mtu anashiriki na wengine. Ufalme hauna kabisa usemi kama huu ama kanuni kama hii. Kama mtu anaweza kusalimika hatimaye, ni kwa sababu amefikia mahitaji ya Mungu, na kama mtu hawezi hatimaye kubaki katika kipindi cha pumziko, ni kwa sababu mtu huyu hamtii Mungu na hajakidhi mahitaji ya Mungu. Kila mtu ana hatima inayofaa. Hatima hizi zinaamuliwa kulingana na asili ya kila mtu na hazihusiani kabisa. Mwenendo ovu wa mtoto hauwezi kuhamishwa kwa wazazi wake, na haki ya mtoto haiwezi kushirikishwa wazazi wake. Mwenendo ovu wa mzazi huwezi kuhamishwa kwa watoto wake, na haki ya mzazi haiwezi kushirikishwa watoto wake. Kila mtu anabeba dhambi zake husika, na kila mtu anafurahia bahati yake husika. Hakuna anayeweza kuchukua ya mwingine. Hii ni haki. Kwa mtazamo wa mwanadamu, iwapo wazazi wanapata bahati nzuri, watoto wao pia wanaweza, na watoto wakifanya maovu, wazazi wao lazima walipie dhambi zao. Huu ni mtazamo wa mwanadamu na njia ya mwanadamu ya kufanya vitu. Si mtazamo wa Mungu. Matokeo ya kila mtu yanaamuliwa kulingana na asili inayotoka kwa mwenendo wao, na daima yanaamuliwa inavyofaa. Hakuna awezaye kubeba dhambi za mwingine; hata zaidi ya hayo, hakuna anayeweza kupokea adhabu badala ya mwingine. Hii ni thabiti. Malezi ya upendo ya mzazi kwa watoto wake hayamaanishi kwamba anaweza kufanya matendo ya haki badala ya watoto wake, wala upendo wenye utiifu wa mtoto kwa wazazi wake haumaanishi kwamba anaweza kufanya matendo ya haki badala ya wazazi wake. Hiyo ndiyo maana ya kweli ya maneno haya, “Basi kutakuwa na watu wawili shambani; mmoja wao atachukuliwa, na mwingine kuachwa. Wanawake wawili watakuwa wakisaga katika kisiagi; mmoja atachukuliwa, na mwingine kuachwa.” Hakuna anayeweza kuwaingiza watoto wake watenda maovu rahani kwa msingi wa upendo wao wa kina kwa watoto wao, wala hakuna anayeweza kumwingiza mke wake (ama mume) rahani kwa sababu ya mwenendo wao wa haki. Hii ni kanuni ya utawala; hakuwezi kuwa na ubaguzi kwa mtu yeyote. Wanaotenda haki ni wanaotenda haki, na watenda maovu ni watenda maovu. Watenda haki watasalimika, na watenda maovu wataangamizwa. Watakatifu ni watakatifu; wao si wachafu. Wachafu ni wachafu, na hawana sehemu yoyote takatifu. Watu wote waovu wataangamizwa, na watu wote wa haki watasalimika, hata kama watoto wa watenda maovu wanafanya matendo ya haki, na hata kama wazazi wa mtu wa haki wanafanya matendo maovu. Hakuna uhusiano kati ya mume anayeamini na mke asiyeamini, na hakuna uhusiano kati ya watoto wanaoamini na wazazi wasioamini. Ni aina mbili zisizolingana. Kabla ya kuingia rahani, mtu ana jamaa wa kimwili, lakini baada ya mtu kuingia rahani, mtu hana jamaa wa

kimwili tena wa kuzungumzia. Wanaofanya wajibu wao na wasiofanya ni adui, wanaompenda Mungu na wanaomchukia Mungu ni wapinzani. Wanaoingia rahani na wale ambao wameangamizwa ni aina mbili ya viumbe wasiolingana. Viumbe wanaotimiza wajibu wao watasalimika, na viumbe wasiotimiza wajibu wao wataangamizwa; zaidi ya hayo, hii itadumu milele. Je, unampenda mume wako ili kutimiza wajibu wako kama kiumbe? Je, unampenda mke wako ili kutimiza wajibu wako kama kiumbe? Je, wewe ni mtiifu kwa wazazi wako wasioamini ili kutimiza wajibu wako kama kiumbe? Mtazamo wa mwanadamu wa kumwamini Mungu ni sahihi ama la? Mbona unamwamini Mungu? Unataka kupata nini? Unampenda Mungu jinsi gani? Wasioweza kutimiza wajibu wao kama viumbe na hawawezi kufanya juhudi nzima wataangamizwa. Watu leo wana mahusiano ya kimwili miongoni mwao, na pia ushirikiano wa damu, lakini baadaye hii yote itavunjwa. Waumini na wasioamini hawalingani ila wanapingana. Walio rahani wanaamini kwamba kuna Mungu na wanamtii Mungu. Wasiomtii Mungu wote watakuwa wameangamizwa. Familia hazitakuwa tena duniani; kunawezaje kuwa na wazazi na watoto ama mahusiano kati ya waume na wake? Kutoambatana kati ya imani na kutoamini kutakuwa kumevunja haya mahusiano ya kimwili!

Awali hakukuwa na familia miongoni mwa binadamu; mwanamume na mwanamke tu walikuwepo—aina mbili tofauti za wanadamu. Hakukuwa na nchi, sembuse familia, lakini kwa sababu ya upotovu wa mwanadamu, watu wa aina yote walijipanga katika koo binafsi, baadaye kukua kwa nchi na mataifa. Nchi na mataifa haya yalikuwa na familia ndogo binafsi, na kwa namna hii watu wa aina yote walisambazwa miongoni mwa jamii mbalimbali kulingana na tofauti ya lugha na mipaka igawayo. Kwa kweli, bila kujali idadi ya jamii zilizo duniani, binadamu wana babu mmoja pekee. Mwanzoni, kulikuwa na watu wa aina mbili tu, na aina hizi mbili zilikuwa mwanamume na mwanamke. Hata hivyo, kwa sababu ya maendeleo ya kazi ya Mungu, kupita kwa historia na mabadiliko ya kijiografia, kwa viwango mbalimbali aina hizi mbili za watu ziliendelezwa kuwa watu wa aina nyingine zaidi. Mwishowe, bila kujali idadi ya jamii zilizo katika binadamu, binadamu wote bado ni viumbe wa Mungu. Bila kujali jamii ambayo watu wako ndani, wote ni viumbe Wake; wote ni vizazi vya Adamu na Hawa. Hata kama hawajatengenezwa na mikono ya Mungu, ni vizazi vya Adamu na Hawa, ambao Mungu Mwenyewe aliumba. Bila kujali aina ambayo watu wako ndani, wote ni viumbe Wake; kwa sababu ni wa binadamu, ambao uliumbwa na Mungu, hatima yao ni hiyo ambayo binadamu wanapaswa kuwa nayo, na wamegawanywa kulingana na kanuni zinazopanga binadamu. Hiyo ni kusema kwamba, watenda maovu na wenye haki, hata hivyo, ni viumbe. Viumbe wafanyao maovu wataangamizwa hatimaye, na viumbe wafanyao matendo ya haki watasalimika. Huu ni mpangilio unaofaa sana wa viumbe wa aina hizi mbili. Watenda maovu hawawezi, kwa sababu ya kutotii kwao, kukataa kwamba ni viumbe wa Mungu lakini wameporwa na Shetani na hivyo

hawawezi kuokolewa. Viumbe wa mwenendo wa haki hawawezi kutegemea ukweli kwamba watasalimika kukataa kwamba wameumbwa na Mungu na bado wamepokea wokovu baada ya kupotoshwa na Shetani. Watenda maovu ni viumbe wasiomtii Mungu; ni viumbe ambao hawawezi kuokolewa na tayari wameporwa na Shetani. Watu wanaotenda maovu ni watu pia; ni watu waliopotoshwa mno na watu wasioweza kuokolewa. Jinsi walivyo viumbe pia, watu wa mwenendo wa haki pia wamepotoshwa, lakini ni watu walio tayari kuacha tabia yao potovu na wanaweza kumtii Mungu. Watu wa mwenendo wa haki hawajajaa haki; badala yake, wamepokea wokovu na kuacha tabia yao potovu kumtii Mungu; watashikilia msimamo huo mwishowe, lakini hii si kusema kwamba hawajapotoshwa na Shetani. Baada ya kazi ya Mungu kuisha, miongoni mwa viumbe Wake wote, kutakuwa na wale watakoangamizwa na wale watakosalimika. Huu ni mwelekeo usioepukika wa kazi Yake ya usimamizi. Hakuna anayeweza kuyakataa haya. Watenda maovu hawawezi kusalimika; wanaomtii na kumfuata Mungu hadi mwishowe hakika watasalimika. Kwa sababu kazi hii ni ya usimamizi wa binadamu, kutakuwa na wale watakoabaki na wale watakoondolewa. Haya ni matokeo tofauti ya watu wa aina tofauti, na hii ndiyo mipango inayofaa zaidi ya viumbe Wake. Mpango wa mwisho wa Mungu kwa mwanadamu ni kugawa kwa kuzivunja familia, kuyavunja mataifa na kuivunja mipaka ya kitaifa. Ni moja isiyo na familia na mipaka ya kitaifa, kwani mwanadamu, hata hivyo, ni wa babu mmoja na ni kiumbe wa Mungu. Kwa ufupi, viumbe wafanyao maovu wataangamizwa, na viumbe wanaomtii Mungu watasalimika. Kwa njia hii, hakutakuwa na familia, hakutakuwa na nchi na hasa hakutakuwa na mataifa katika pumziko la baadaye; binadamu wa aina hii ni aina takatifu kabisa ya binadamu. Adamu na Hawa waliumbwa awali ili mwanadamu aweze kutunza mambo yote duniani; mwanadamu awali alikuwa bwana wa vitu vyote. Nia ya Yehova ya kumuumba mwanadamu ilikuwa kumruhusu mwanadamu kuwa duniani na pia kutunza vitu vyote duniani, kwani mwanadamu awali hakuwa amepotoshwa na pia hakuweza kutenda maovu. Hata hivyo, baada ya mwanadamu kupotoshwa, hakuwa mtunzaji wa vitu vyote tena, na madhumuni ya wokovu wa Mungu ni kurejesha kazi hii ya mwanadamu, kurejesha ufahamu wa awali wa mwanadamu na utii wake wa awali; binadamu rahani watakuwa picha halisi ya matokeo ambayo kazi ya Mungu ya wokovu inatarajia kufikia. Ingawa hayatakuwa tena maisha kama yale ya bustani ya Edeni, kiini chake kitakuwa sawa; binadamu hawatakuwa tu nafsi yake ya awali isiyo potovu, lakini badala yake binadamu waliopotoshwa na kisha kupata wokovu. Watu hawa waliopata wokovu hatimaye (yaani, baada ya kazi Yake kuisha) wataingia rahani. Vivyo hivyo, matokeo ya wale walioadhibiwa pia yote yatafichuliwa mwishowe, na wataangamizwa tu baada ya kazi Yake kuisha. Hii ni kusema kwamba baada ya kazi Yake kuisha, watendao maovu na wale waliookolewa wote watafichuliwa, kwani kazi ya kufichua watu wa aina zote (bila kujali iwapo ni watenda maovu ama waliookolewa) itatekelezwa kwa watu wote wakati huo huo. Watenda maovu wataondolewa, na wale wanaoweza kubaki

watafichuliwa wakati huo huo. Kwa hivyo, matokeo ya watu wa aina zote yatafichuliwa wakati huo huo. Hataliruhusu kwanza kundi la watu waliookolewa kuingia rahani kabla ya kuweka kando watenda maovu na kuwahukumu au kuwaadhibu kidogo kidogo; ukweli kwa kweli si hivyo. Wakati watenda maovu wanaangamizwa na waliosalimika wanaingia rahani, kazi Yake katika ulimwengu mzima itakuwa imemalizika. Hakutakuwa na utaratibu wa kipaumbele miongoni mwa wale wanaopata baraka na wale wanaopata taabu; wanaopokea baraka wataishi milele, na wanaopata taabu wataangamia milele. Hizi hatua mbili za kazi zitakamilika wakati huo huo. Ni hasa kwa sababu kuna watu wasiotii ndiyo maana haki ya watu wanaotii itafichuliwa, na ni hasa kwa sababu kuna wale waliopokea baraka ndiyo maana taabu ya wale wanaotenda maovu kwa sababu ya mwenendo wao mbovu itafichuliwa. Kama Mungu hakufichua watenda maovu, hao watu wanaomtii Mungu kwa dhati hawangeona jua; kama Mungu hangewapelekea wanaomtii katika hatima inayofaa, wasiomtii Mungu hawangeweza kupata adhabu wanayostahili. Huu ndio mwendo wa kazi Yake. Kama hangefanya kazi hii ya kuadhibu maovu na kutuza mazuri, viumbe Wake hawangeweza kuingia hatima zao husika. Mwanadamu aingiapo rahani, watenda maovu wataangamizwa, binadamu wote wataingia katika njia sahihi, na watu wa kila aina watakuwa na aina yao kulingana na kazi wanayopaswa kufanya. Hii tu ndiyo itakuwa siku ya binadamu kupumzika na mwenendo usioepukika wa maendeleo ya binadamu, na wakati tu binadamu wataingia rahani ndipo utimilifu mkubwa na wa mwisho wa Mungu utamalizika; hii itakuwa tamati ya kazi Yake. Hii kazi itamaliza maisha ya uharibifu ya kimwili ya binadamu, na itamaliza maisha ya binadamu potovu. Kutoka hapa binadamu wataingia katika ulimwengu mpya. Ingawa mwanadamu anaishi kimwili, kuna tofauti kubwa kati ya kiini cha maisha yake na kiini cha maisha ya binadamu wapotovu. Maana ya kuwepo kwake na maana ya kuwepo kwa binadamu wapotovu pia ni tofauti. Ingawa haya si maisha ya mtu wa aina mpya, inaweza kusemwa kuwa maisha ya binadamu ambao wamepata wokovu na maisha yenye ubinadamu na busara kurejeshwa. Hawa ni watu ambao hawakumtii Mungu wakati mmoja, na ambao walishindwa na Mungu wakati mmoja na baadaye kuokolewa na Yeye; hawa ni watu waliomwaibisha Mungu na baadaye wakamshuhudia. Uwepo wao, baada ya kupitia na kuendelea kuishi baada ya jaribio Lake, ni uwepo wa maana kubwa zaidi; ni watu waliomshuhudia Mungu mbele ya Shetani; ni watu wanaofaa kuishi. Watakaoangamizwa ni watu wasioweza kumshuhudia Mungu na hawafai kuishi. Maangamizo yao yatakuwa kwa sababu ya mwenendo wao mwovu, na maangamizo ni hatima yao bora zaidi. Mwanadamu aingiapo baadaye katika ulimwengu mzuri, hakutakuwa na mahusiano kati ya mume na mke, kati ya baba na binti ama kati ya mama na mwana wa kiume ambayo mwanadamu anafikiria atapata. Wakati huo, mwanadamu atafuata aina yake, na familia itakuwa tayari imevunjwa. Baada ya kushindwa kabisa, Shetani hatawasumbua binadamu tena, na mwanadamu hatakuwa tena na tabia potovu ya kishetani. Wale watu wasiotii watakuwa wameangamizwa tayari, na wale watu wanaotii pekee

ndio wataishi. Na basi familia chache sana zitasalimika bila kuharibika; mahusiano ya kimwili yatawezaje kuweko? Maisha ya kimwili ya zamani ya mwanadamu yatapigwa marufuku kabisa; mahusiano ya kimwili yatawezaje kuweko kati ya watu? Bila tabia potovu ya kishetani, maisha ya watu hayatakuwa tena maisha ya zamani ya siku zilizopita, lakini badala yake maisha mapya. Wazazi watapoteza watoto, na watoto watapoteza wazazi. Waume watapoteza wake, na wake watapoteza waume. Watu sasa wana mahusiano ya kimwili miongoni mwao. Wakati wote watakuwa wameingia rahani hakutakuwa na mahusiano ya kimwili tena. Binadamu kama hawa tu ndio watakuwa wa haki na watakatifu, binadamu kama hawa tu ndio watamwabudu Mungu.

Mungu aliumba binadamu na Akawaweka duniani, ambao Amewaongoza mpaka siku ya leo. Kisha Akaokoa binadamu na kuhudumu kama sadaka ya dhambi kwa binadamu. Mwishowe lazima bado ashinde binadamu, aokoe binadamu kabisa na kuwarejesha kwa mfano wao wa awali. Hii ndiyo kazi Amekuwa akifanya kutoka mwanzo hadi mwisho—kurejesha mwanadamu kwa sura yake halisi na kwa mfano wake wa awali. Ataanzisha ufalme Wake na kurejesha mfano wa awali wa mwanadamu, kumaanisha kwamba Atarejesha mamlaka Yake duniani na kurejesha mamlaka Yake miongoni mwa viumbe vyote. Mwanadamu alipoteza moyo wake wa kumcha Mungu baada ya kupotoshwa na Shetani na kupoteza kazi ambayo kiumbe mmoja wa Mungu anapaswa kuwa nayo, kuwa adui asiyemtii Mungu. Mwanadamu alimilikiwa na Shetani na kufuata amri za Shetani; hivyo Mungu hakuwa na njia ya kufanya kazi miongoni mwa viumbe Wake, na hakuweza zaidi kuwafanya viumbe Wake kumcha. Mwanadamu aliumbwa na Mungu, na anapaswa kumwabudu Mungu, lakini mwanadamu kwa kweli alimpuuza Mungu na kumwabudu Shetani. Shetani alikuwa sanamu katika moyo wa mwanadamu. Hivyo Mungu alipoteza nafasi yake katika moyo wa mwanadamu, kusema kwamba Alipoteza maana ya uumbaji Wake wa mwanadamu, na ili kurejesha maana ya uumbaji Wake wa mwanadamu lazima arejeshe mfano wa awali wa mwanadamu na kumtoa mwanadamu tabia yake potovu. Ili kumrejesha mwanadamu kutoka kwa Shetani, lazima Amwokoe mwanadamu kutoka kwa dhambi. Kwa njia hii tu ndiyo Anaweza kurejesha mfano wa awali wa mwanadamu polepole na kurejesha kazi halisi ya mwanadamu, na mwishowe kurejesha ufalme Wake. Maangamizo ya mwisho ya wale wana wa uasi pia yatafanywa ili kumruhusu mwanadamu kumwabudu Mungu vizuri zaidi na kuishi duniani vizuri zaidi. Kwa sababu Mungu alimuumba mwanadamu, Atamfanya mwanadamu amwabudu; kwa sababu Anataka kurejesha kazi halisi ya mwanadamu, Atairejesha kabisa, na bila ughushi wowote. Kurudisha mamlaka Yake kunamaanisha kumfanya mwanadamu amwabudu na kumfanya mwanadamu amtii; kunamaanisha kwamba Atamfanya mwanadamu aishi kwa sababu Yake na kufanya adui zake waangamie kwa sababu ya mamlaka Yake; kunamaanisha kwamba Atafanya kila sehemu Yake kuendelea miongoni mwa binadamu na bila upinzani wowote wa mwanadamu. Ufalme Anaotaka kuanzisha ni ufalme Wake

Mwenyewe. Binadamu Anaotaka ni wale wanaomwabudu, wale wanaomtii kabisa na wana utukufu Wake. Asipookoa binadamu wapotovu, maana ya uumbaji Wake wa mwanadamu hautakuwa chochote; Hatakuwa na mamlaka yoyote miongoni mwa mwanadamu, na ufalme Wake hautaweza kuweko tena duniani. Asipoangamiza wale adui wasiomtii, Hataweza kupata utukufu Wake wote, wala Hataweza kuanzisha ufalme Wake duniani. Hizi ndizo ishara za ukamilishaji wa kazi Yake na ishara za ukamilishaji wa utimilifu Wake mkubwa; kuangamiza kabisa wale miongoni mwa binadamu wasiomtii, na kuwaleta wale waliokamilika rahani. Wakati binadamu wamerejeshwa katika mfano wake wa awali, wakati binadamu wanaweza kutimiza kazi yao husika, kuwa na nafasi zao wenyewe na kutii mipango yote ya Mungu, Mungu atakuwa amepata kundi la watu duniani wanaomwabudu, na Atakuwa pia Ameanzisha ufalme duniani unaomwabudu. Atakuwa na ushindi wa milele duniani, na wale wanaompinga wataangamia milele. Hii itarejesha nia Yake ya asili ya kumuumba mwanadamu; itarejesha nia Yake ya kuumba vitu vyote, na pia itarejesha mamlaka Yake duniani, mamlaka Yake miongoni mwa vitu vyote na mamlaka yake miongoni mwa adui Zake. Hizi ni ishara za ushindi Wake wote. Tangu sasa na kwendelea binadamu wataingia katika raha na kuingia katika maisha yafuatayo njia sahihi. Mungu pia ataingia katika raha ya milele na mwanadamu na kuingia katika maisha ya milele yanayoshirikisha Mungu na mwanadamu. Uchafu na kutotii duniani vitatoweka, na pia maombolezo duniani. Wote walio duniani wanaompinga Mungu hawatakuweko. Mungu na wale Aliowaokoa pekee ndio watabaki; viumbe Wake tu ndio watabaki.

Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani IV (1994 hadi 1997, 2003 hadi 2005)

Kufikia Utakapouona Mwili wa Kiroho wa Yesu, Mungu Atakuwa Ametengeneza Upya Mbingu na Dunia

Je, ungependa kumwona Yesu? Je, ungependa kuishi na Yesu? Je, ungependa kuyasikia maneno yaliyonenwa na Yesu? Iwapo ni hivyo, basi utakaribishaje kurudi kwa Yesu? Je, uko tayari kabisa? Utakaribisha kurudi kwa Yesu kwa namna gani? Nafikiri kuwa kila ndugu anayemfuata Yesu angependa kumpa Yesu makaribisho mazuri. Lakini Je, mmewazia hili: Mtamjua Yesu kweli Atakaporejea? Je, mtaelewa kweli kila kitu Atakachosema? Je, mtakubali kweli, bila masharti, kila kazi ambayo Anafanya? Wale wote ambao wamesoma Biblia wanajua kuhusu kurudi kwa Yesu, na wale wote ambao wamesoma Biblia wanangoja kwa makini kuja Kwake. Nyote mmetazamia kufika kwa wakati huo, na uaminifu wenu ni wa kusifika, imani yenu kweli ni ya kuleta wivu, lakini mnatambua kuwa mmefanya kosa kuu? Yesu Atarejea kwa namna gani? Mnaamini kuwa Yesu Atarudi juu ya wingu jeupe, lakini Nawauliza: Wingu hili jeupe linaashiria nini? Na kwa kuwa wafuasi wengi wa Yesu wanangoja kurejea Kwake,

Atashuka miongoni mwa watu wapi? Iwapo ninyi ni wa kwanza kati ya wale ambao Yesu Atawashukia, Je, wengine hawataona jambo hili kama lisilo la haki sana? Najua kuwa nyinyi mna ukweli mkubwa na utiifu kwa Yesu, lakini mmewahi kukutana na Yesu? Mnajua tabia Yake? Mmewahi kuishi na Yeye? Mnaelewa kiasi gani kumhusu kwa kweli? Wengine watasema kuwa maneno haya yanawaweka katika tatizo gumu. Watasema, “Nimesoma Biblia kuanzia mwanzo hadi mwisho mara nyingi sana. Nitakosaje kumwelewa Yesu? Usijali kuhusu tabia ya Yesu—najua hata rangi ya nguo Alizopenda kuvaa. Je, haushushi hadhi yangu ukisema simwelewi?” Napendekeza kuwa usiyapinge masuala haya; ni heri utulie na kufanya ushirika juu ya maswali yafuatayo: Kwanza, unajua uhalisi ni nini, na nadharia ni nini? Pili, unajua dhana ni nini, na ukweli ni nini? Tatu, unajua kile kinachowazwa na kile kilicho halisi?

Watu wengine wanakataa ukweli kuwa hawamwelewi Yesu. Ilhali Nasema hammwelewi hata kidogo, na hamwelewi hata neno moja la Yesu. Hiyo ni kwa sababu kila mmoja wenu anamfuata Yeye kwa sababu ya matukio ya Biblia, kwa sababu ya yale yaliyosemwa na wengine. Hamjawahi kumwona Yesu, sembuse kuishi na Yeye, na hata hamjapata kushinda na Yeye hata kwa muda mfupi. Hivyo, je, kuelewa kwenu kuhusu Yesu sio nadharia pekee? Je, si kuelewa kwenu kunakosa uhakika? Labda watu wengine wameiona picha ya Yesu, ama wengine wametembea nyumbani kwa Yesu kibinafsi. Labda wengine wamegusa mavazi ya Yesu. Ilhali kuelewa kwako kumhusu bado ni kwa nadharia na ila si kwa vitendo, hata kama umeonja chakula kilicholiwa na Yesu binafsi. Haijalishi ni hali ipi, hujawahi kumwona Yesu, na hujawahi kuwa pamoja na Yeye katika hali ya kimwili, na hivyo, kuelewa kwako kumhusu Yesu kutabaki kuwa nadharia tupu daima ambako hakuna ukweli. Pengine maneno Yangu yana uvutio mdogo kwako, lakini Nakuuliza hivi: Ingawa labda umesoma maandishi mengi yaliyoandikwa na mwandishi unayempenda, je, unaweza kumwelewa kikamilifu bila kuwahi kukaa na yeye kwa muda? Je, unajua tabia yake ilivyo? Je, unajua ni maisha ya aina gani anayoishi? Unajua chochote kuhusu hali ya hisia zake? Huwezi hata kumwelewa kikamilifu mwanadamu unayempenda, sasa utawezaje kumwelewa Yesu Kristo? Kila kitu unachoelewa kumhusu Yesu kimejaa mawazo na dhana, na hakina ukweli wowote wala uhalisi. Kinanuka, na kimejaa mwili. Kuelewa kwa aina hii kutakuwezesha vipi kustahili kukaribisha kurejea kwa Yesu? Yesu hatawakaribisha wale waliojawa na mawazo na dhana za mwili. Wale wasiomwelewa watafaa vipi kuwa waumini Wake?

Je, mngependa kujua kiini cha sababu ya Mafarisayo kumpinga Yesu? Je, mnataka kujua dutu ya Mafarisayo? Walikuwa wamejawa na mawazo makuu kuhusu Masiha. Kilicho zaidi, waliamini tu kuwa Masiha angekuja, ilhali hawakutafuta ukweli wa uzima. Na hivyo, hata leo bado wanamngoja Masiha, kwani hawana maarifa ya njia ya uzima, na hawajui ukweli ni nini. Ni vipi, hebu nielezeni, watu wapumbavu, wakaidi na washenzi kama hawa wangeweza kupata

baraka za Mungu? Wangeweze kumwona Masiha? Walimpinga Yesu kwa sababu hawakujua mwelekeo wa kazi ya Roho Mtakatifu, kwa sababu hawakuijua njia ya ukweli uliozungumziwa na Yesu, na zaidi, kwa sababu hawakumwelewa Masiha. Na kwa kuwa hawakuwa wamewahi kumwona Masiha na hawakuwa wamewahi kuwa pamoja na Masiha, walifanya kosa la kuning'inia bila mafanikio kwa jina la Masiha huku wakipinga dutu ya Masiha kwa kila njia iwezekanayo. Mafarisayo hawa kwa dutu walikuwa wakaidi, wenye kiburi na hawakutii ukweli. Kanuni ya imani yao kwa Mungu ni: Haijalishi mahubiri Yako ni makubwa vipi, haijalishi mamlaka Yako ni makubwa vipi, Wewe si Kristo iwapo Huitwi Masiha. Je, maoni haya si ya upuuzi na ya kudhihaki? Nawauliza tena: Je, si rahisi sana kwenu kufanya makosa ya Mafarisayo wa mbeleni zaidi, kwa kuwa hamna ufahamu hata kidogo kumhusu Yesu? Je, unaweza kuitambua njia ya ukweli? Je, unaweza kutoa uhakika kweli kuwa hutampinga Kristo? Je, una uwezo wa kuifuata kazi ya Roho Mtakatifu? Kama hujui iwapo utampinga Kristo, basi Nasema kuwa tayari unaishi kwenye ukingo wa kifo. Wale wote ambao hawakumfahamu Masiha walikuwa na uwezo wa kumpinga Yesu, wa kumkataa Yesu, wa kumpaka Yeye tope. Watu wote wasiomwelewa Yesu wako na uwezo wa kumkana, na kumtusi. Zaidi, wako na uwezo wa kuona kurejea kwa Yesu kama uwongo wa Shetani, na watu zaidi watamshutumu Yesu aliyerudi kwa mwili. Je, haya yote hayawafanyi muogope? Mtakachokumbana nacho kitakuwa kumkufuru Roho Mtakatifu, kuharibiwa kwa maneno ya Roho Mtakatifu kwa makanisa, na kukataliwa kwa dhara ya yale yote ambayo yamedhihirishwa na Yesu. Mnaweza kupata nini kutoka kwa Yesu kama mmetatizwa kwa namna hii? Mtaielewaje kazi ya Yesu atakaporudi kwa mwili kwa wingu jeupe, kama mnakataa katakata kuona makosa yenu? Nawaambieni hili: Watu wasiokubali ukweli, ilhali wanangoja kufika kwa Yesu juu ya wingu jeupe kwa upofu, kwa hakika watamkufuru Roho Mtakatifu, na ni kundi ambalo litaangamizwa. Mnatamani tu neema ya Yesu, na kutaka tu kufurahia ulimwengu wa mbinguni wenye raha, ilhali hamjawahi kutii maneno yaliyonenwa na Yesu, na hamjawahi kupokea ukweli utakaonyeshwa na Yesu atakaporudi katika mwili. Mtashikilia nini badala ya ukweli wa kurejea kwa Yesu juu ya wingu jeupe? Je, ni ukweli ambao ndani yake mnashinda mkitenda dhambi, na kisha kuzikiri, tena na tena? Mtatoa nini kama kafara kwa Yesu Anayerejea juu ya wingu jeupe? Je, ni miaka ya kazi ambayo mnajiinua nayo? Ni nini mtakachoinua kumfanya Yesu Anayerejea kuwaamini? Je, ni hiyo asili yenu ya kiburi, ambayo haitii ukweli wowote?

Uaminifu wenu uko kwa maneno pekee, maarifa yenu ni ya kiakili tu na ya dhana, kazi yenu ni kwa sababu ya kupata baraka za mbinguni, na kwa hivyo imani yenu inafaa kuwa vipi? Hata leo, bado mnapuuza kila neno la ukweli. Hamjui Mungu ni nini, hamjui Kristo ni nini, hamjui jinsi ya kumcha Yehova, hamjui jinsi ya kuingia katika kazi ya Roho Mtakatifu, na hamjui jinsi ya kutofautisha kati ya kazi ya Mungu Mwenyewe na uongo wa mwanadamu.

Unajua tu kukashifu neno lolote la ukweli linaloelezwa na Mungu lisilolingana na mawazo yako. Unyenyekevu wako uko wapi? Utiifu wako uko wapi? Uaminifu wako uko wapi? Tamaa yako ya kupata ukweli iko wapi? Uchaji Mungu wako uko wapi? Nawaambieni, wale wanaoamini katika Mungu kwa sababu ya ishara hakika ni kikundi ambacho kitapata kuangamizwa. Wale wasio na uwezo wa kukubali maneno ya Yesu Ambaye Amerudi kwa mwili kwa hakika ni vizazi vya kuzimu, vizazi vya malaika mkuu, kikundi ambacho kitakabiliwa na kuangamizwa kwa milele. Watu wengi wanaweza kukosa kujali kuhusu kile Ninachosema, lakini bado Nataka kumwambia kila anayedaiwa kuwa mtakatifu wa Mungu anayemfuata Yesu kwamba, mtakapona Yesu Akishuka kutoka juu mbinguni juu ya wingu jeupe kwa macho yenu wenyewe, huu ndio utakuwa mwonekano wa umma wa Jua la haki. Pengine huo utakuwa wakati wa furaha kubwa kwako, ilhali lazima ujue kuwa wakati utakaposhuhudia Yesu Akishuka kutoka mbinguni ndio pia wakati ambapo utaenda chini kuzimu kuadhibiwa. Huo ndio utakuwa wakati wa mwisho wa mpango wa Mungu wa usimamizi na ndio utakuwa wakati ambapo Mungu atawatunukia wazuri na kuwaadhibu waovu. Kwani hukumu ya Mungu itakuwa imeisha kabla ya mwanadamu kuona ishara, wakati kuna onyesho la ukweli tu. Wale wanaokubali ukweli na hawatafuti ishara, na hivyo wametakaswa, watakuwa wamerudi mbele za kiti cha enzi cha Mungu na kuingia katika kumbatio la Muumba. Ni wale tu ambao wanashikilia imani kwamba “Yesu Asiyeshuka juu ya wingu jeupe ni Kristo wa uongo” watakaliwa na adhabu ya milele, kwani wanaamini tu katika Yesu ambaye Anaonyesha ishara, lakini hawamkubali Yesu Anayetangaza hukumu kali na Anatoa njia ya kweli ya uzima. Na hivyo itakuwa tu kuwa Yesu Atawashughulikia tu Atakaporejea wazi wazi juu ya wingu jeupe. Ni wakaidi sana, wanajiamini sana, wenye kiburi sana. Wapotovu kama hawa watatunukiwa vipi na Yesu? Kurejea kwa Yesu ni wokovu mkuu kwa wale ambao wana uwezo wa kuukubali ukweli, lakini kwa wale wasioweza kuukubali ukweli ni ishara ya kuhukumiwa. Mnafaa kuchagua njia yenu wenyewe, na hampaswi kukufuru Roho Mtakatifu na kuukataa ukweli. Hampaswi kuwa wajinga wala watu walio na kiburi, lakini watu ambao wanatii uongozi wa Roho Mtakatifu na wanangoja kwa hamu na kuutafuta ukweli; kwa njia hii tu ndiyo mtapata kufaidika. Nawashauri mtembee katika njia ya kuamini katika Mungu kwa uangalifu. Msiwe wepesi wa kuamua mambo bila kuzingatia suala zima; kilicho zaidi, msiwe wenye kuchukulia mambo bila uzito na wenye msiofikiria katika imani yenu kwa Mungu. Mnafaa kujua kwamba, angalau, wale wanaoamini Mungu wanafaa kuwa wanyenyekevu na wenye kucha. Wale ambao wamesikia ukweli ilhali wanaudharau ni wajinga na wapumbavu. Wale ambao wameusikia ukweli ilhali bila kujali wanaamua mambo bila kuzingatia kila kitu ama kuukashifu wamejawa na kiburi. Hakuna anayeamini katika Yesu anastahili kuwalaani au kuwahukumu wengine. Nyote mnafaa kuwa watu walio wenye mantiki na wanaoukubali ukweli. Pengine, baada ya kusikia njia ya kweli na kusoma neno la uzima, unaamini kuwa neno moja tu kati ya maneno haya elfu kumi ndiyo

yanayolingana na dhana zako na Biblia, na kisha unafaa kuendelea kutafuta katika moja kati ya elfu kumi ya maneno haya. Bado Nawashauri muwe wanyenyekevu, msijiamini sana, na msijiinue juu sana. Moyo wako ukiwa na uchaji mdogo kama huu kwa Mungu, utapata mwanga mkuu. Ukichunguza kwa makini na kurudia kutafakari maneno haya, utapata kuelewa iwapo ni ukweli au la, na iwapo ni ya uzima au la. Pengine, baada ya kusoma tu sentensi chache, watu wengine watacashifu kwa upofu maneno haya, wakisema, “Hiki sicho chochote ila nuru kiasi ya Roho Mtakatifu,” ama, “Huyu ni Kristo wa uongo ambaye amekuja kuwadanganya watu.” Wale wanaosema vitu kama hivyo wamepofushwa na ujinga! Unaelewa kiasi kidogo sana kuhusu kazi na hekima ya Mungu, na Nakushauri uanze tena kutoka mwanzo! Hamfai kuyakashifu kwa upofu maneno yaliyonenwa na Mungu kwa sababu ya kutokea kwa Makristo wa uongo katika siku za mwisho, na hampaswi kuwa watu wanaomkufuru Roho Mtakatifu kwa sababu mnaogopa kudanganywa. Je, hiyo haitakuwa hali kubwa ya kuhuzunisha? Iwapo, baada ya uchunguzi mwingi, bado unaamini kuwa maneno haya si ukweli, si njia, na si maonyesho ya Mungu, basi utaadhibiwa hatimaye, na kuwa bila baraka. Iwapo huwezi kukubali ukweli kama huu ulionenwa wazi sana na kwa kawaida sana, basi wewe si ni asiyefaa kwa wokovu wa Mungu? Je, wewe si mtu ambaye hana bahati ya kutosha kurejea mbele za kiti cha enzi cha Mungu? Waza kuhusu hili! Usiwe mwenye pupa wala wa haraka, na usiichukulie imani kwa Mungu kama mchezo. Fikiria kwa ajili ya hatima yako, kwa ajili ya matarajio yako, kwa ajili ya maisha yako, na usifanye mchezo na nafsi yako. Je, unaweza kuyakubali maneno haya?

Wale Ambao Hawalingani na Kristo Hakika Ni Wapinzani wa Mungu

Watu wote wana tamaa ya kuona uso wa kweli wa Yesu na wote hutaka kuwa pamoja Naye. Naamini kuwa hakuna mmoja wa ndugu au dada anayeweza kusema kwamba yeye hana nia ya kumwona au kuwa pamoja na Yesu. Kabla ya nyinyi kumwona Yesu, yaani, kabla ya nyinyi kumwona Mungu Aliye kwenye mwili, mnaweza kuwa na mawazo mengi, kwa mfano, kuhusu sura ya Yesu, njia Yake ya kuzungumza, njia Yake ya maisha, na kadhalika. Hata hivyo, wakati mmemwona hasa, mawazo yenu yatabadilika haraka. Ni kwa nini? Je, mnataka kujua? Hata ingawa fikira za mwanadamu hakika haziwezi kupuuzwa, haikubaliki hata zaidi kwa mwanadamu kubadilisha kiini cha Kristo. Nyinyi mnamchukua Kristo kama asiyekufa au mhenga, lakini hakuna anayemchukulia kama mwanadamu wa kawaida mwenye kiini kitakatifu. Kwa hivyo, wengi wa wale ambao wanatamani usiku na mchana kumwona Mungu ni hasa maadui wa Mungu na hawapatani na Mungu. Je, haya si makosa kwa upande wa mwanadamu? Hata sasa bado mnadhani kwamba imani yenu na uaminifu umetosha kuwafanya mstahili kuona uso wa Kristo, lakini Mimi Nawasihi kujihami kwa mambo zaidi yaliyo na umuhimu! Hii ni kwa

maana katika wakati uliopita, uliopo na ujao, wengi wa wale ambao hupatana na Kristo wameanguka au wataanguka; wao wote wamechukua jukumu la Mafarisayo. Sababu yenu ya kushindwa ni nini? Ni kwa sababu hasa katika fikra zenu kuna Mungu mkubwa, Atamanikaye. Lakini ukweli si kama vile mwanadamu atakavyo. Kristo si mkubwa tu, bali Yeye ni mdogo hasa; Yeye si mtu tu, bali ni mtu wa kawaida; Hana uwezo wa kupaa mbinguni tu, bali hana pia uhuru wa kuzunguka ardhini. Na kwa hivyo, watu humtendea kama mtu wa kawaida; wao humtendea kikawaida wanapokuwa pamoja naye, na kusema maneno kiholela Kwake, wakati huu wote wakingojea kurudi kwa “Kristo wa kweli.” Mnamchukua Kristo aliyekuja tayari kama mtu wa kawaida na neno Lake kama lile la mtu wa kawaida. Kwa hivyo, hamjapata chochote kutoka kwa Kristo na badala yake mmeonyesha ubaya wenu kwenye mwangaza kabisa.

Kabla ya kuwasiliana na Kristo, unaweza kuamini kwamba tabia yako imebadilishwa kabisa, kwamba wewe ni mfuasi mwaminifu wa Kristo, na kwamba wewe unastahili kupokea baraka za Kristo zaidi. Pia kwamba, kwa kuwa umesafiri njia nyingi, umefanya kazi nyingi, na kuleta matunda mengi, hivyo ni lazima utakuwa mtu anayepata taji mwishowe. Hata hivyo kuna ukweli ambao huenda hujui: Tabia potovu na uasi na upinzani wa mwanadamu huonekana wazi mara tu anapomwona Kristo, na uasi na upinzani unaoonekana wakati huu kwa hakika na kamilifu kuliko wakati mwingine wote. Ni kwa sababu Kristo ni Mwana wa Adamu—Mwana wa Adamu aliye na ubinadamu wa kawaida—kwamba mwanadamu hamwogopi wala kumheshimu. Ni kwa sababu Mungu anaishi katika mwili ndio maana uasi wa mwanadamu hufichuliwa kikamilifu na kwa uwazi sana. Kwa hivyo Nasema kwamba kuja kwake Kristo kumechimbua uasi wote wa wanadamu na kutupa asili ya mwanadamu katika afueni ya ghafla. Huku kunaitwa “kumvuta chui mkubwa kutoka mlimani” na “kumvuta mbwa mwitu kutoka pangoni pake.” Je, unathubutu kusema kwamba wewe ni mwaminifu kwa Mungu? Je, unathubutu kusema kwamba wewe huonyesha utiifu kamili kwa Mungu? Je, unathubutu kusema kwamba wewe si muasi? Wengine watasema: Kila wakati ambao Mungu ananiweka katika mazingira mapya, mimi daima hutii na silalamiki na aidha siweki fikra zozote juu ya Mungu. Wengine watasema: Kazi zozote nilizopewa na Mungu mimi hufanya kadri ya uwezo wangu na kamwe mimi si mvivu. Kama ndivyo hali, Nawauliza hivi: Je, mnaweza kulingana na Kristo wakati mnaishi pamoja naye? Na ni kwa muda gani nyinyi mnaweza kulingana na Yeye? Siku moja? Siku mbili? Saa moja? Saa mbili? Imani yenu inaweza kuwa ya kustahili sifa, lakini hamna uthabiti wa kutosha. Wakati unaishi na Kristo kwa kweli, kujidai kwako na kujigamba kwako kutawekwa wazi kwa maneno na matendo yako kidogo kidogo, na hivyo ndivyo tamaa yako ya kupindukia, na akili yako isiyotii na kutoridhika kwako kutafichuka kwa kawaida. Mwishowe, kiburi chako kitakuwa kikubwa zaidi, hadi wakati wewe utazozana sana na Kristo kama maji na moto, na basi asili yako itawekwa wazi kabisa. Wakati huo, fikra zako haziwezi

kufichika tena, malalamiko yako, pia, yataonekana kwa ghafla, na ubinadamu wako duni utakuwa wazi kabisa. Hata hivyo, hata wakati huo, utaendelea kukana uasi wako mwenyewe, ukiamini kwamba badala yake kwamba Kristo kama huyu si rahisi kukubaliwa na mwanadamu, ni mwingi wa madai kwa binadamu, na ungetii kikamilifu kwake kama Yeye angekuwa tu Kristo mwenye huruma zaidi. Mnaamini kwamba daima kuna sababu ya haki ya uasi wenu, na kwamba nyinyi mnamwasi tu baada ya Kristo amewafikisha hatua fulani. Kamwe hamjawahi kufikiri kwamba mmekosa kumchukulia Kristo kama Mungu na katika nia ya kumtii. Badala yake, wewe kwa ukaidi unasisitiza Kristo afanye kazi Yake kulingana na matakwa yako, na punde ambapo kuna jambo lolote ambamo Hafanyi hivyo, basi unaamini kwamba Yeye si Mungu bali ni mwanadamu. Je, si kuna wengi kati yenu ambao wameridhika na Yeye katika hali hii? Ni nani huyo mnayemwamini hata hivyo? Na ni jinsi gani mnatafuta?

Kila mara mnataka kumwona Kristo, lakini Nawasihi msijipandishe hadhi hivyo; kila mtu anaweza kumwona Kristo, lakini Nasema hakuna ambaye ni wa kufaa kumwona Kristo. Kwa sababu asili ya binadamu imejazwa na uovu, kiburi, na uasi, wakati unapomwona Kristo, asili yako itakuharibu na itakuhukumu hadi kufa. Ushirika wako na ndugu (au dada) huenda usionyeshe mengi kukuhusu wewe, lakini si rahisi hivyo unaposhiriki na Kristo. Wakati wowote, fikira zako zinaweza kukita mizizi, kiburi chako kianze kuchipuka, na uasi wako kuzaa mitini. Unawezaje kufaa kushiriki na Kristo na ubinadamu kama huo? Je, kweli unaweza kumchukua Yeye kama Mungu kila wakati wa kila siku? Je, kweli utakuwa na hali halisi ya utiifu kwa Mungu? Mnamuabudu Mungu mkubwa ndani ya mioyo yenu kama Yehova wakati mnamchukua Kristo anayeonekana kama mwanadamu. Hisia zenu ni duni mno na ubinadamu wenu ni wa hali ya chini! Hamwezi kumfikiria Kristo kama Mungu milele; ni mara chache tu, mnapotaka, ndio mnamshika na kumwabudu kama Mungu. Hii ndiyo sababu Ninasema nyinyi si waumini wa Mungu, ila kikundi cha washirika ambao wanaopigana dhidi ya Kristo. Hata watu ambao huonyesha wema kwa wengine hulipwa, lakini Kristo, ambaye amefanya kazi ya namna hiyo kati yenu, hajapokea upendo wa Mungu au fidia na utii wake. Je, hili si ni jambo la kusikitisha moyo?

Inaweza kuwa kwamba katika miaka yako yote ya imani katika Mungu, kamwe hujamlaani mtu yeyote wala kufanya tendo mbaya, lakini katika ushirika wako na Kristo, huwezi kusema ukweli, kutenda kwa uaminifu, au kutii neno la Kristo; basi, Ninasema kwamba wewe ndiye mtu mwovu zaidi na mwenye nia mbaya zaidi duniani. Unaweza kuwa mkunjufu na mwaminifu mno kwa jamaa zako, marafiki, mke (au mume), wanao na mabinti, na wazazi, na kamwe huwatumii wengine vibaya, lakini kama huwezi kulingana na kupatana na Kristo, basi hata ukitumia vitu vyako vyote kuwasaidia majirani zako au kulinda vizuri baba yako, mama, na wanakaya, Ningesema kwamba wewe bado ni mwovu, na zaidi ya hayo aliyejaa hila za ujanja. Usifikiri,

kwamba wewe unalingana na Kristo kwa sababu tu unapatana na wengine au unafanya baadhi ya matendo mema. Je, unafikiri kwamba nia yako ya huruma inaweza kupata baraka kutoka Mbinguni kwa ujanja? Je, unafikiri kwamba matendo machache mema yanaweza kubadilishwa na utii wako? Hakuna hata mmoja wenu anaweza kukubali kushughulikiwa na kupogolewa, na wote wanaona vigumu kukubali ubinadamu wa kawaida wa Kristo, hata hivyo siku zote mnatangaza utiifu wenu kwa Mungu. Imani kama yenu italeta adhabu ya kufaa. Wacheni kujihusisha katika ndoto za ajabu na kutaka kumwona Kristo, kwa maana nyinyi ni wadogo sana katika kimo, kiasi kwamba nyinyi hata hamstahili kumwona. Wakati umeuwacha kabisa uasi wako na unaweza kupatana na Kristo, wakati huo Mungu Atakuonekana kwa kawaida. Iwapo utaenda kumwona Mungu kabla ya kupogolewa au kupitia hukumu, basi bila shaka utakuwa mpinzani wa Mungu na utakuwa katika njia ya kuangamizwa. Asili ya mwanadamu kwa kawaida ina uhasama kwa Mungu, kwa kuwa watu wote wamepotosha kabisa na shetani. Hakuna kizuri kinachoweza kupatikana kwa mtu kujaribu kushirikiana na Mungu kutokana na upotovu wake. vitendo na maneno yake kwa hakika vitafichua upotovu wake kila wakati; na katika kushirikiana na Mungu, uasi wake utafichuka katika vipengele vyote. Binadamu, kwa kutojua anakuja anampinga Kristo, kumdanganya Kristo, na kumtelekeza Kristo; hili litakapofanyika, mwanadamu atakuwa katika hali ya hatari zaidi na, hili likiendelea, atapata adhabu.

Baadhi ya watu wanaweza kuamini kwamba, kama kushirikiana na Mungu ni hatari sana, basi huenda likawa jambo la busara zaidi kukaa mbali na Mungu. Ni nini watu kama hawa wanaweza kupokea? Je, wanaweza kuwa waaminifu kwa Mungu? Hakika, kushirikiana na Mungu ni kugumu sana, lakini hiyo hasa ni kwa sababu mwanadamu amepotoka na si kwa sababu Mungu hawezi kushiriki naye. Ingekuwa bora kwenu kuweka juhudi zaidi kwa ukweli wa kuzijua nafsi zenu. Mbona hamjapata fadhili kwa Mungu? Kwa nini tabia zenu ni chukizo sana Kwake? Kwa nini maneno yenu yanachochea chuki Yake? Punde ambapo mmeonyesha uaminifu kidogo, nyinyi mnajisifu wenyewe, na mnadai malipo kwa ajili ya mchango mdogo; nyinyi huwadharau wengine wakati nyinyi mnaonyesha utiifu kidogo, na kumdharau Mungu baada ya kufanya kazi ndogo. Mnataka utajiri, zawadi na pongezi kwa ajili ya kumpokea Mungu. Nyoyo zenu huumwa wakati mnatoa sarafu moja au mbili; wakati mnatoa kumi, mnataka kubarikiwa na kutendewa kwa heshima. Ubinadamu kama wenu kweli ni wa kukera kuzungumziwa au kusikizwa. Kuna chochote kinachostahili sifa katika maneno na matendo yenu? Wale ambao wanatekeleza wajibu wao na wale wasiofanya; wale ambao huongoza na wale ambao hufuata; wale wanaompokea Mungu na wale wasiompokea; wale wanaotoa na wale wasiotoa; wale wanaohubiri na wale ambao hupokea neno, na kadhalika; watu wote kama hawa hujisifu wenyewe. Je, hamuoni hili likiwa la kuchekesha? Mkijua vyema kwamba mnamwamini

Mungu, hata hivyo ninyi hamwezi kulingana na Mungu. Kweli mnajua vyema kwamba hamstahili hata kidogo. Je, hamhisi kuwa hisia yenu imepunguka kiasi kwamba hamwezi tena kujizuia? Na hisia kama hii, mnastahili vipi kushirikiana na Mungu? Je, kufikia hapa nyinyi hamjionei hofu? Tabia yenu tayari imepunguka kiasi kwamba hamwezi kulingana na Mungu. Hali ikiwa hivi, je, imani yenu si ya kucheakesha? Imani yenu si ya kipuuzi? Ni jinsi gani utashughulikia maisha yako ya baadaye? Ni jinsi gani utachagua njia ya kutembelea?

Wengi Wanaitwa, Lakini Wachache Wanachaguliwa

Nimewatafuta wengi duniani wawe wafuasi Wangu. Kati ya hawa wafuasi wote, kuna wale wanaohudumu kama makuhani, wale wanaoongoza, wanaojumuisha wana, wanaojumuisha watu, na wale wanaotoa huduma. Nawagawa katika makundi haya tofauti kwa msingi wa uaminifu wanaonionyesha. Wakati wanadamu wote wameainishwa kulingana na aina zao, yaani, asili ya kila aina ya mwanadamu inapowekwa wazi, basi Nitamhesabu kila mwanadamu miongoni mwa aina yake kamili na kuweka kila aina katika nafasi yake kamili ili Nikamilishe lengo Langu la ukombozi wa mwanadamu. Moja baada ya mwingine, Nayaita makundi ya wale Ningependa kuwaokoa kurejea katika nyumba Yangu, kisha Nawaruhusu watu hawa wote wakubali kazi Yangu katika siku za mwisho. Wakati uo huo, Nawaainisha wanadamu kulingana na aina, kisha Namtunuku au kumwadhibu kila mmoja kulingana na matendo yake. Hizi ndizo hatua zinazojumuisha kazi Yangu.

Sasa Naishi duniani na Naishi miongoni mwa wanadamu. Wanadamu wote wanashuhudia kazi Yangu na kutazama matamko Yangu, na pamoja na hili Natoa ukweli kwa kila mfuasi Wangu ili waweze kupokea uzima kutoka Kwangu na hivyo apate njia anayoweza kufuata. Kwa maana Mimi ni Mungu, mpaji wa uhai. Katika miaka mingi ya kazi Yangu, mwanadamu amepokea vitu vingi na kujinyima vitu vingi, lakini bado Nasema kuwa mwanadamu haniamini kikamilifu. Kwa maana mwanadamu anakubali kijuujuu tu kuwa Mimi ni Mungu lakini hakubaliani na ukweli Ninaounena, sembuse kuweka ukweli katika matendo Ninavyohitaji kwake. Hiyo ni kusema, mwanadamu anakubali tu uwepo wa Mungu, lakini sio ule wa ukweli; mwanadamu hukubali tu uwepo wa Mungu, lakini sio wa uzima; mwanadamu anakubali tu jina la Mungu, lakini sio kiini Chake. Kutokana na ari yake, mwanadamu amekuwa chukizo mbele Zangu. Kwa kuwa mwanadamu anatumia tu maneno yanayofurahisha masikio kunihadaa, na hakuna anayeniabudu kwa moyo wa kweli. Maneno yenu yanabeba majaribu ya ibilisi. Na maneno yenu ni yenye kiburi kupindukia, ni vile tu kama yamesemwa na malaika mkuu. Zaidi ya hayo, matendo yenu yamechakaa; tamaa zenu zisizo na kiasi na nia zenu zenye tamaa ni za kukera zikisikizwa. Nyote mmegeuka nondo katika nyumba Yangu, vyombo vya kukataliwa na chukizo. Kwa maana hapana kati yenu ambao ni wapenda ukweli, bali ni wanadamu

wanaopenda baraka tu, walio na matamano ya kupaa mbinguni, na ya kumwona Kristo anapoonyesha nguvu Zake duniani. Lakini mmewahi kuwaza jinsi mwanadamu kama ninyi, aliyepotoka sana, na asiyejua kabisa Mungu ni nini, angestahili kumfuata Mungu? Mnawezaje kupaa mbinguni? Mnawezaje kustahili kuuona uzuri wa ukuu usio na kifani? Vinywa vyenu vimejaa maneno ya uongo na uchafu, usaliti na kiburi. Kamwe hamjawahi kunena maneno ya ukweli Kwangu, wala maneno matakatifu, wala maneno ya kunitii baada ya kulipitia neno Langu. Hatimaye, hii imani yenu ni ya aina gani? Nyoyo zenu zimejaa tamaa na mali, mawazo yenu yamejaa mali ya kilimwengu. Kila siku, mnafanya hesabu jinsi mtakavyofaidika kutoka Kwangu, mkihesabu kiasi cha mali na vitu vya kidunia mlivyopata kutoka Kwangu. Kila siku, mnangoja baraka zaidi ziwashukie ili muweze kufurahia, hata zaidi na vyema zaidi, vitu zaidi vya raha. Vile vilivyo katika mawazo yenu kila wakati si Mimi, wala ukweli utokao Kwangu, bali ni mume (mke), mwanao, bintiyo au mlacho na kuvaa, na vile mtakavyoburudika na starehe nzuri zaidi. Hata mlishindilie tumbo lenu kwa vyakula hadi pomoni, je, si nyinyi bado ni zaidi ya maiti tu? Hata wakati ambapo, kwa nje, mnavalia mavazi ya kupendeza sana, si nyinyi bado ni maiti inayotembea isiyo na uhai? Mnafanya kazi kwa bidii kwa ajili ya tumbo lenu mpaka mnapotokwa na mvi, ilhali hakuna aliye tayari kuutoa unywele mmoja kwa ajili ya kazi Yangu. Mnasafiri kila mara, mnafanya kazi na kupiga bongo kwa ajili ya miili yenu, na kwa sababu ya watoto wenu, ilhali hakuna yeyote anayeshughulika wala kufikiria kuhusu mapenzi Yangu. Ni nini ambacho bado mnatarajia kufaidi kutoka Kwangu?

Katika kufanya kazi Yangu, kamwe Siharakishwi. Hata mwanadamu anifuata vipi, Mimi hufanya kazi Yangu kulingana na kila hatua, kulingana na mpango Wangu. Kwa hivyo, hata ingawa mnaweza kuasi dhidi Yangu sana, bado Sisimamishi kazi Yangu na Ninaendelea kunena maneno Ninayotaka kunena. Nawaita katika nyumba Yangu wale Niliowajaalia kulisikiliza neno Langu, kisha Nawaweka wote wanaotii na kulitarajia neno Langu mbele ya kiti Changu cha enzi. Wale wanaolisaliti neno Langu, wale wasiotii na kujisalimisha Kwangu, na wale wanaonipinga kwa wazi, watatupwa kando wakingoja adhabu ya mwisho. Wanadamu wote wanaishi katika upotovu na chini ya mkono wa yule mwovu, kwa hivyo sio wengi wanaonifuata wako na hamu ya ukweli kwa hakika. Hiyo ni kusema, wengi wao hawaniabudu kwa moyo wa kweli au kwa ukweli, lakini wanajaribu kupata uaminifu Wangu kupitia ufisadi, uasi na njia nyinginezo danganyifu. Ni kwa sababu hii ndiyo Nasema: Wengi wameitwa, lakini ni wachache wamechaguliwa. Wote walioitwa wametoka kupindukia na wanaishi katika enzi sawa, lakini wale waliochaguliwa ni lile kundi tu la wanaoamini na kuukubali ukweli na kuutia ukweli katika matendo. Wanadamu hawa ni sehemu ndogo tu ya wanadamu wote, na kutoka miongoni mwa wanadamu hawa Nitapata utukufu zaidi. Ukijipima kulingana na maneno haya, je, mnajua kama nyinyi mumo kati ya waliochaguliwa? Je, hatima yenu itakuwa namna gani?

Tayari Nimeshasema kuwa wale wanaonifuata ni wengi lakini wanaonipenda kwa moyo wa kweli ni wachache. Huenda ikawa wengine wanasema, “Ningeweza kulipa gharama kubwa kiasi hicho kama ningekuwa sikupendi Wewe? Ningefuata mpaka hatua hii kama singekuwa nakupenda?” Kwa hakika, unazo sababu nyingi, kwa hakika, upendo wako ni mkubwa sana, lakini umuhimu wa mapenzi yako Kwangu ni nini? “Upendo,” kama unavyoitwa, unaashiria hisia safi isiyo na dosari, ambapo unatumia moyo wako kupenda, kuhisi, na kuwa na mawazo. Katika upendo hakuna masharti, hakuna vizuizi na hakuna kutenga. Katika upendo hakuna shaka, hakuna uongo na hakuna ujanja. Katika upendo hakuna mabadilishano na hakuna kitu kisicho safi. Ukipenda, basi hutadanganya, hutalalamika, hutalalamika, hutaasi kulazimisha au kutafuta kupata kitu au kupata kiwango fulani. Ukipenda, basi utajinyima bila kusononeka na kuvumilia hali ngumu, na utaambatana na Mimi. Utaacha kila kitu chako kwa sababu Yangu, utaacha familia yako, siku zako za baadaye, ujana wako, na ndoa yako. La sivyo, basi upendo wako haungekuwa upendo hata kidogo, bali ungekuwa uongo na usaliti! Upendo wako ni upendo wa aina gani? Je, ni upendo wa kweli? Je, ni wa uongo? Umejinyima kiasi gani? Umejitolea kiasi gani? Je, Nimepata upendo kiasi gani kutoka kwako? Je, unajua? Mioyo yenu imejaa maovu, usaliti na uongo na hivyo kuna kiwango kipi cha uchafu katika upendo wenu? Mnafikiri kuwa mmeacha ya kutosha kwa ajili Yangu; mnafikiri kuwa upendo wenu Kwangu tayari umetosha. Ila ni kwa nini basi maneno yenu na matendo yenu huambatana na uasi na uongo daima? Mnanifuata, ilhali hamkubali neno Langu. Je, hili linachukuliwa kama upendo? Mnanifuata, kisha mnanitenga na kunitupa kando. Je, huu unachukuliwa kama upendo? Mnanifuata, na bado mko na shaka na Mimi. Je, huu unachukuliwa kama upendo? Mnanifuata, ilhali hamkubali kuwepo Kwangu. Je, huu ni upendo? Mnanifuata, ilhali hamnitendei vile Ninavyopaswa kutendewa na mnafanya mambo yawe magumu Kwangu katika kila hatua. Je, hili linachukuliwa kama upendo? Mnanifuata, na bado mnanichukua kama mjinga na kunidanganya Mimi katika kila jambo. Je, hili linachukuliwa kama upendo? Mnanihudumia, na bado hamnichi. Je, hili linachukuliwa kama upendo? Mnanipinga katika kila hali na kila jambo. Je, yote haya yanachukuliwa kama upendo? Mmejinyima mengi, huu ni ukweli, lakini bado hamjawahi kutenda Ninayowaagiza mfanye. Je, huu unaweza kuchukuliwa kama upendo? Uchunguzi wa makini unaashiria kuwa hamna upendo Kwangu ndani yenu. Baada ya miaka mingi sana ya kazi na maneno yote mengi Niliyosambaza, ni kiasi kipi mlichopokea kwa hakika? Je, hili halistahili kuangaliwa tena kwa makini? Nawaonya: Wale Niwaitao Kwangu sio wale ambao hawajawahi kupotoshwa, bali wale Ninaowachagua ni wale wanaonipenda kwa ukweli. Kwa hivyo, mnapaswa kuwa makini na maneno na matendo yenu, na mchunguze maazimio na mawazo yenu ili vitu hivi visije vikavuka mipaka. Wakati huu wa siku za mwisho, fanyeni jitihada ili muonyeshe mapenzi yenu Kwangu, isije ghadhabu yangu ikabaki kwenu milele!

Unapaswa Kutafuta Njia ya Uwiano na Kristo

Nimefanya kazi kubwa miongoni mwa binadamu, na maneno ambayo Nimeeleza wakati huu yamekuwa mengi. Maneno haya ni kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu, na yalikuwa yanaeleza ili binadamu aweze kulingana na Mimi. Ilhali Nimewapokea watu wachache tu duniani ambao wanalingana na Mimi, na hivyo Nimesema kwamba binadamu hathamini maneno Yangu, kwa kuwa binadamu halingani na Mimi. Kwa njia hii, kazi ambayo Naifanya sio tu kwa ajili ya mwanadamu aweze kuniabudu; muhimu zaidi, ni kwa ajili ya mwanadamu aweze kulingana na Mimi. Watu, ambao wamepotoshwa, wote huishi katika mtego wa Shetani, wao kuishi katika mwili, kuishi katika tamaa za ubinafsi, na hakuna hata mmoja kati yao anayelingana na Mimi. Kuna wale ambao wanasema kwamba wao wanalingana na Mimi, lakini ambao wote huabudu sanamu zisizo yakini. Ingawa wanakubali jina Langu kama takatifu, wao hutembea kwenye njia ambazo huenda kinyume na Yangu, na maneno yao yamejaa kiburi na kujiamini, kwa sababu, katika mizizi, wote wananipinga na hawalingani Nami. Kila siku wao hutafuta dalili Yangu katika Biblia, na kupata vifungu “vinavyofaa” hapa na pale wanavyovisoma bila kukoma, na ambavyo wao hukariri kama maandiko. Hawajui jinsi ya kulingana na Mimi, hawajui maana ya kuwa katika uadui na Mimi, na wanasoma tu maandiko kwa upofu. Wao huzuia ndani ya Biblia na Mungu asiye yakini ambaye hawajawahi kumwona, na hawana uwezo wa kumwona, na wao huitoa tu na kuiangazia wakati wao wa ziada. Wao wanaamini kuwepo Kwangu tu ndani ya eneo la Biblia. Kwa fikira zao, Mimi ni sawa na Biblia; bila Biblia Mimi sipo, na bila Mimi hakuna Biblia. Wao hawatilii maanani kuwepo Kwangu au matendo, lakini badala yake hujishughulisha na umakini mno na maalum kwa kila neno la Maandiko, na wengi wao hata huamini kwamba Mimi sipaswi kufanya jambo lolote Nipendalo kufanya ila tu kama lilitabiriwa na Maandiko. Wao hutia umuhimu mwingi sana kwa Maandiko. Inaweza kusemwa kwamba wao huona maneno na maonyesho yakiwa muhimu mno, kwa kiasi kwamba wao hutumia mistari ya Biblia kupima kila neno Ninalolisema, na kunilaani Mimi. Wanalotafuta si njia ya uwiano na Mimi, au njia ya uwiano na ukweli, lakini njia ya uwiano na maneno ya Biblia, na wanaamini kwamba chochote ambacho hakiambatani na Biblia, bila ubaguzi, si kazi Yangu. Je, si watu wa namna hiyo ni wazawa watiifu wa Mafarisayo? Mafarisayo Wayahudi walitumia sheria ya Musa kumhukumu Yesu. Hawakutafuta uwiano na Yesu wa wakati huo, bali waliifuata sheria kwa makini, kwa kiasi kwamba wao hatimaye walimpiga misumari Yesu asiye na hatia juu ya msalaba, baada ya kumshitaki Yeye kwa kukosa kufuata sheria za Agano la Kale na kutokuwa Masihi. Kiini chao kilikuwa ni nini? Haikuwa kwamba hawakutafuta njia ya uwiano na ukweli? Walitamani na kutilia maanani mawazo yao na kila neno la Maandiko, bila kuyajali mapenzi Yangu na hatua na mbinu za kazi Yangu. Hawakuwa watu waliotafuta ukweli, ila walikuwa watu walioshikilia maneno kwa ugumu;

hawakuwa watu walioamini katika Mungu, bali walikuwa watu walioamini katika Biblia. Kimsingi, walikuwa walinzi wa Biblia. Ili kulinda maslahi ya Biblia, na kuzingatia hadhi ya Biblia, na kulinda sifa za Biblia, wao walitenda kiasi kwamba walimsulubisha Yesu mwenye huruma msalabani. Haya walifanya tu kwa ajili ya kuitetea Biblia, na kwa ajili ya kudumisha hali ya kila neno la Biblia katika mioyo ya watu. Hivyo waliona ni heri kuyaacha maisha yao ya baadaye na sadaka ya dhambi kwa sababu ya kumhukumu Yesu, ambaye hakuwa Anazingatia kanuni za Maandiko, mpaka kifo. Je hawakuwa watumishi kwa kila mojawapo ya maneno ya Maandiko?

Na je watu leo? Kristo amekuja kutoa ukweli, lakini wanaona ni afadhali wao kumfukuza Yeye kutoka kati ya wanadamu ili wapate kuingia mbinguni na kupokea neema. Wanaona ni afadhali kabisa kukataa kuja kwa ukweli, ili kulinda maslahi ya Biblia, na ni afadhali kumtundika Kristo ambaye Alirudi kwa mwili kwa misumari msalabani tena ili kuhakikisha kuwepo kwa Biblia milele. Jinsi gani mwanadamu anaweza kupokea wokovu Wangu, wakati moyo wake una nia mbaya namna hiyo, na asili yake inanipinga Mimi? Mimi huishi miongoni mwa wanadamu, ilhali bado wanadamu hawajui kuhusu kuwepo Kwangu. Ninapoangaza mwanga Wangu juu ya wanadamu, bado yeye hana ufahamu kuhusu kuwepo Kwangu. Wakati Ninatoa ghadhabu Yangu juu ya wanadamu, wao hukanusha kuwepo Kwangu kwa nguvu kubwa zaidi. Binadamu hutafuta uwiano na maneno, na Biblia, ilhali bado hakuna mwanadamu hata mmoja huja Kwangu kutafuta njia ya uwiano na ukweli. Binadamu huniheshimu sana Nikiwa mbinguni, na kujishughulisha hasa na kuwepo Kwangu mbinguni, ilhali hakuna anayenijali Nikiwa katika mwili, kwa maana Mimi Ninayeishi miongoni mwa wanadamu sina umuhimu kwao hata kidogo. Wale ambao hutafuta tu uwiano na maneno ya Biblia, na ambao hutafuta tu uwiano na Mungu asiye yakini, mbele Yangu ni fidhuli. Hiyo ni kwa sababu wanachokiabudu ni maneno yaliyokufa, na Mungu Aliye na uwezo wa kuwapa hazina isiyoambilika. Wanachoabudu ni Mungu anayedhibitiwa na mtu, na ambaye hayuko. Ni nini, basi, ambacho watu wa namna hiyo wanaweza kupokea kutoka Kwangu? Mwanadamu ni kiumbe duni sana kiasi kwamba maneno hayawezi kueleza hali yake. Wale wanaonipinga, wanaofanya madai yasiyo na kipimo dhidi Yangu, wasio na upendo kwa ukweli, wanaoniasi—wangepewezeje kulingana na Mimi?

Wale wanaonipinga ni wale ambao hawalingani na Mimi. Vile vile wale wasiopenda ukweli, na wale wanaoniasi ndio walio wapinzani Wangu zaidi na hawalingani na Mimi. Wale wote ambao hawalingani na Mimi Nawawasilisha mikononi mwa yule mwovu. Ninawaacha wao kwa upotovu wa yule mwovu, Nawaachilia huru ili wafichue maovu yao, na hatimaye kuwakabidhi kwa yule mwovu ili waliwe. Mimi Sijali ni watu wangapi wananiabudu, ambayo ni kusema, Sijali ni watu wangapi wanaamini ndani Yangu. Kinachonijalisha ni watu wangapi wanalingana na Mimi. Hiyo ni kwa sababu wote wasiolingana na Mimi ni wale waovu

wanaonisaliti; wao ni adui Zangu, Nami “Sitawatunza” adui Zangu katika nyumba Yangu. Wale ambao wanalingana na Mimi watanitumikia milele katika nyumba Yangu, na wale wanaojiweka katika uadui na Mimi watateseka milele katika adhabu Yangu. Wale wanaojali tu kuhusu maneno ya Biblia, wasiojali kuhusu ukweli au kutafuta nyayo Zangu—wao wananipinga, kwa kuwa wao wananizuilia Mimi kulingana na Biblia, na kuniwekea vizuizi ndani ya na Biblia, na hivyo ni wa kukufuru pakubwa dhidi Yangu. Jinsi gani watu wa aina hii wanaweza kuja mbele Zangu? Wao hawatilii maanani matendo Yangu, au mapenzi Yangu, au ukweli, badala yake wanashikilia maneno, maneno yanayoua. Jinsi gani watu kama hao wanaweza kulingana na Mimi?

Nimeeleza maneno mengi sana, na pia nimeeleza mapenzi Yangu na tabia, lakini hata hivyo, bado watu hawana uwezo wa kunijua Mimi na kuniamini. Au, inaweza kusemwa, bado hawana uwezo wa kunitii. Wale wanaoishi katika Biblia, wale wanaoishi katika sheria, wale wanaoishi juu ya msalaba, wale ambao wanaishi kwa mujibu wa mafundisho, wale wanaoishi miongoni mwa kazi Ninayofanya leo—yupi kati yao analingana na Mimi? Ninyi mnafikiria tu kupokea baraka na tuzo, na hamjawahi kamwe kufikiria jinsi ya kulingana na Mimi, au jinsi ya kujizuia wenyewe kutoka katika uadui na Mimi. Nimeaibishwa sana na nyinyi, kwa kuwa Nimewapa mengi sana, ilhali Mimi Nimepokea kidogo sana kutoka kwenu. Udanganyifu wenu, kiburi chenu, tamaa yenu, tamaa yenu yenye fujo, usaliti wenu, kuasi—lipi kati ya haya linaweza kujificha kutoka kwa macho Yangu? Ninyi mnanitendea hobela hobela, mnanidanganya Mimi, mnanitusi, mnanibembeleza, mnanilazimisha na kupata sadaka kutoka Kwangu kwa nguvu—ni jinsi gani tabia ya kudhuru kama hii itaepuka ghadhabu Yangu? Udhalimu wenu ni thibitisho la uadui wako Kwangu, na ni thibitisho la uwiano wenu na Mimi. Kila mmoja wenu anaamini mwenyewe akilingana na Mimi, lakini ikiwa ni hivyo, basi ni kwa nani ushahidi huu dhahiri unatumika? Mnaamini wenyewe kwamba mnao ukweli wa juu sana na uaminifu Kwangu. Mnafikiri kwamba nyinyi ni wema sana, wenye huruma sana, na mmetoa sana Kwangu. Mnafikiri kwamba mmefanya vya kutosha kwa ajili Yangu. Bado hamjawahi kulinganisha imani hizi dhidi ya tabia zenu wenyewe? Nasema mmejaa mengi ya kiburi, tamaa nyingi, wingi wa uzembe; hila mnayotumia kunidanganya ni janja sana, na mna mengi ya nia ya kudharau na mbinu ya kudharau. Uaminifu wenu pia ni mdogo, bidii yenu pia ni ndogo, na dhamiri yako hata haipo zaidi. Kuna mabaya mengi sana katika nyoyo zenu, na hakuna mtu anayeepuka kuathiriwa na hila yenu, hata Mimi mwenyewe. Mnanifungia nje kwa ajili ya watoto wenu, au waume wenu, au kwa ajili ya hifadhi zenu wenyewe. Badala ya kunijali, mnajali familia zenu, watoto wenu, hali yenu, maisha yenu ya baadaye, na kujitosheleza wenyewe. Ni lini mmewahi kuniwaza Mimi mnapozungumza au kutenda? Wakati hali ya hewa ni baridi, mawazo yenu hurejea kwa watoto wenu, waume wenu, wake wenu, au wazazi wenu. Wakati hali ya hewa ni ya joto, hata

Siwezi kupata nafasi katika mawazo yenu pia. Unapotekeleza wajibu wako, wewe huwaza tu kuhusu maslahi yako mwenyewe, ya usalama wako mwenyewe binafsi, ya watu wa familia yako. Ni nini umewahi kufanya kwa ajili Yangu? Ni lini umeweza kuwaza kunihusu Mimi? Ni lini umewahi kujitoa mwenyewe, kwa gharama yoyote, kwa ajili Yangu na kazi Yangu? Uko wapi ushahidi wa uwiano wako na Mimi? Uko wapi ukweli wa uaminifu wako kwa ajili Yangu? Uko wapi ukweli wa utiifu wako Kwangu? Ni lini mujibu wako hujakuwa kwa sababu ya kupokea baraka Zangu? Mnanilaghai na kunidanganya Mimi, mnacheza na ukweli na kuficha kuwepo kwa kweli, na kuisaliti dutu ya ukweli, na mnajiweka wenyewe kwa uadui kama huu na Mimi. Basi, ni nini kinawangoja katika siku za usoni? Ninyi mnatafuta tu uwiano na Mungu asiye yakini, na kutafuta tu imani zisizo yakini ilhali ninyi hulingani na Kristo. Si uovu wenu utapata adhabu kama ile wanayostahili waovu? Wakati uo huo, mtagundua kuwa hakuna mtu yeyote asiyelingana na Kristo atakayeepuka siku ya ghadhabu, na mtagundua ni aina gani ya adhabu italetwa juu ya wale walio katika uadui na Kristo. Siku hiyo itakapofika, ndoto yenu ya kubarikiwa kwa imani yenu katika Mungu na kupata kuingia mbinguni, yote itakatizwa. Lakini, hata hivyo, si hivyo kwa wale ambao wanalingana na Kristo. Ingawa wao wamepoteza sana, ingawa wamekabiliwa na mengi ya ugumu wa maisha, watapokea urithi wote ambao Nimeutoa kwa ajili ya mwanadamu. Hatimaye, mtalewa kwamba Mimi tu ndiye Mungu mwenye haki, na kwamba ni Mimi tu Niliye na uwezo wa kuwachukua binadamu mpaka kwenye hatima yao yenye kupendeza.

Je, Wewe Ni Muumini wa Kweli wa Mungu?

Huenda ikawa safari yako ya imani katika Mungu imekuwa ndefu zaidi ya mwaka mmoja au miwili, na labda kwa maisha yako umestahimili ugumu mwingi miaka hii yote; au labda haujapitia ugumu na badala yake umepokea neema nyingi. Kuna uwezekano pia kuwa hujapitia ugumu wala kupokea neema, na badala yake umeishi maisha ya kawaida tu. Hiyo haijalishi, kwani wewe bado u mfuasi wa Mungu, kwa hivyo tushirikiane kuhusu mada ya kumfuata Mungu. Lakini, lazima Niwakumbushe wote wanaoyasoma maneno haya kwamba neno la Mungu huelekezwa kwa wale wanaomtambua na wale wanaomfuata Mungu, na sio kwa watu wote wa ulimwengu, wakiwemo wale wasiomtambua Mungu. Ikiwa unaamini kuwa Mungu Anazungumza na halaiki, ya kuwa Anaongelesha watu wote duniani, basi neno la Mungu halitakuwa la mabadiliko kwako. Kwa hivyo, unafaa uyaweke maneno yote karibu na moyo wako, na usijiweke nje ya wigo la maneno haya. Kwa lolote lile, tuzungumze juu ya mambo yanayofanyika katika nyumba yetu.

Mnafaa nyote kufahamu sasa maana kamili ya kumwamini Mungu. Maana ya imani katika Mungu Niliyozungumzia awali inahusiana na kuingia kwenu kwa hali dhahiri. Lakini leo hii si

juu ya hayo. Leo hii Ningependa kuchambua umuhimu wa imani yako katika Mungu. Bila shaka, lengo la jambo hili ni kuwaelekeza kutoka kwenye mabaya; Nisipofanya hivyo, basi hamtawahi kuifahamu sura yako kamili na utakuwa ukijisifu kila mara kuhusu kujitolea kwako na uaminifu wako. Kwa maneno mengine, Nisipoangazia uovu uliomo ndani ya mioyo yenu, basi kila mmoja wenu atajitwika taji kichwani na kujipa utukufu wote. Asili zenu za majivuno na kiburi huwaelekeza kusaliti dhamiri zenu wenyewe, kuasi na kumpinga Kristo, na kufichua uovu wenu, hivyo basi kuleta kwenye mwangaza fikra zenu, mawazo, tamaa nyingi na macho yaliyojaa ulafi. Ilhali mnaendelea kukiri kwamba mtajitolea maisha yenu kwa ajili ya kazi ya Kristo, na mnakariri tena na tena mambo ya kweli yaliyosemwa na Kristo zamani zile. Hii ndiyo “imani” yenu. Hii ndiyo “imani yenu isiyokuwa na doa”. Kwa muda huu wote, Nimemweka mwanadamu katika nidhamu ya hali ya juu. Iwapo uaminifu wako unakuja na nia na masharti, basi ni heri Nisijihusishe na huo mnaoita uaminifu wenu hata kidogo, kwa maana Ninachukia wale hunidanganya kupitia kwa nia zao na kunanihadaa na masharti. Natamani tu mwanadamu awe mwaminifu kabisa Kwangu, na afanye mambo yote kwa ajili ya, na kudhibitisha neno hilo moja: imani. Ninachukizwa na matumizi yenu ya maneno matamu ili Unifurahishe Mimi. Kwa maana daima Mimi napenda mtende pia kwa ukweli mtupu na uwazi na hivyo Ningependa pia mfanye matendo yenu Kwangu kwa imani ya kweli. Inapofika katika swala la imani, watu wengi hufikiri kwamba wanamfuata Mungu kwa sababu wako na imani, la sivyo hawangevumilia mateso hayo. Basi Nakuuliza hivi: Ni kwa nini humheshimu Mungu ilhali unaamini kuwepo Kwake? Ni kwa nini, basi, haumchi Mungu moyoni mwako iwapo unaamini kuwa Mungu Yupo? Unakubali kuwa Kristo ni kupata mwili kwa Mungu, basi ni kwa nini uwe na dharau Kwake? Kwa nini unatenda bila heshima Kwake? Ni kwa nini unamhukumu wazi wazi? Ni kwa nini siku zote unachunguza Yeye anakoenda? Mbona usijisalimishe katika mipango Yake? Ni kwa nini hutendi kulingana na neno Lake? Ni kwa nini unamhadaa na kumpokonya matoleo Yake? Ni kwa nini unazungumza katika nafasi ya Kristo? Ni kwa nini unatoa hukumu ya kubaini iwapo kazi Yake na neno Lake ni ya kweli? Mbona unathubutu kumkufuru Yeye kisiri? Ni mambo haya na mengine ndiyo yanayounda imani yenu?

Kila sehemu ya usemi na tabia zenu hufichua dalili za kutoamini katika Kristo ulizobeba ndani yako. Nia na malengo yenu kwa yale mnayoyafanya yamejaa kutoamini; hata hiyo hisi itokayo kwa macho yenu imetiwa doa na dalili hizi. Kwa maneno mengine, kila mmoja wenu, katika kila dakika ya kila siku, amebeba vipengele vyenu vya kutoamini. Hii ina maana kuwa kila wakati mko katika hatari ya kumsaliti Kristo, kwa maana damu iliyo ndani ya mishipa yenu imechanganyika na kutomwamini Mungu Aliyepata mwili. Kwa hivyo, Ninasema kwamba nyayo mnazoziwacha katika njia ya imani katika Mungu si nyingi. Safari yenu katika njia ya kumwamini Mungu haina msingi mzuri, na badala yake mnaifanya kazi bila ya kujali matokeo

yake. Nyinyi huwa na shaka na neno la Kristo na huwezi kulitia katika matendo mara moja. Hii ndio sababu ya nyinyi kutokuwa na imani katika Kristo, na daima kuwa na fikira kumhusu Kristo ndio sababu nyingine ya nyinyi kutoamini Kristo. Kuwa na shaka kila mara kuhusu kazi ya Kristo, kuacha neno Lake kuangukia sikio lisilosikia, kuwa na maoni kwa kila kazi inayofanywa na Kristo na kutoifahamu vizuri kazi hiyo, kuwa na ugumu wa kutupilia mbali fikira zako hata baada ya nyinyi kupewa sababu za kufanya vile, na kadhalika; hizi zote ni dalili za kutoamini zilizochanganyika ndani ya mioyo yenu. Ingawa mnafuata kazi ya Kristo na kamwe hubaki nyuma, kuna uasi mwingi uliochanganyika ndani ya mioyo yenu. Uasi huu ni doa la uchafu katika imani yenu kwa Mungu. Pengine hamkubaliani na haya, lakini iwapo huwezi kutambua nia yako kutoka kwayo, basi wewe ndiwe utakayeangamia. Kwa maana Mungu hustawisha wale wanaomwamini kwa kweli pekee, wala sio wale walio na shaka na hasa wale wanaomfuata shingo upande licha ya kutowahi kuamini kuwa Yeye ni Mungu.

Watu wengi hawapati shangwe ndani ya ukweli, na vile vile katika hukumu. Badala yake, wao hupata furaha kwa nguvu na mali; watu kama hawa wanaitwa wanaotafuta mamlaka. Wanatafuta tu madhehebu yaliyo na ushawishi duniani na wahubiri na waalimu wanaotoka katika seminari. Hata ingawa wameikubali njia ya ukweli, bado wako na shaka ndani yao na hawawezi kujitolea kikamilifu. Wanazungumzia kujinyima kwa sababu ya Mungu, lakini macho yao yamelenga tu wahubiri wakuu na waalimu, na Kristo anasukumwa pembeni. Mioyo yao imejaa umaarufu, mali na utukufu. Hawaamini kamwe kuwa mtu wa kawaida tu anaweza kuwashinda wengi vile, kwamba mtu asiye wa kutambulika kwa macho tu anaweza kukamilisha watu. Hawaamini kuwa hawa watu wasio na sifa, walio kwenye vumbi na vilima vya samadi ni watu waliochaguliwa na Mungu. Wanaamini kuwa kama watu wale wangekuwa vyombo vya wokovu Wake Mungu, basi mbingu na ardhi zitageuzwa juu na chini na watu wote watacheka kupindukia. Wanaamini kuwa iwapo Mungu atawachagua watu wasio na sifa yoyote wafanywe viumbe kamili, basi wao walio na sifa watakuwa Mungu Mwenyewe. Maoni yao yamechafuliwa na kutoamini; hakika, mbali na kutoamini, wao ni wanyama wasio na maana. Kwa maana wao wanathamini tu nyadhifa, hadhi kuu na mamlaka; wanachokithamini sana ni makundi makuu na madhehebu makuu. Hawana heshima hata kidogo kwa wale wanaoongozwa na Kristo; wao ni wasaliti tu waliomgeuka Kristo, kuugeuka ukweli na uhai.

Unachopendezwa nacho sio unyenyekevu wa Kristo, ila ni wale wachungaji wa uongo wenye umaarufu. Hupendi maarifa au kupendeza kwa Kristo, bali unapenda wale watukutu wanaojihusisha na ulimwengu mchafu. Unauchekelea uchungu wa Kristo asiye kuwa na pahali pa kulaza kichwa Chake, na badala yake unatamani maiti zinazokamata sadaka na kuishi katika uasherati. Hauko tayari kupokea mateso pamoja na Kristo, lakini unakimbilia mikononi mwa wapinzani wa Kristo hata ingawa wanakupa nyama za mwili pekee, barua na udhibiti pekee.

Hata sasa, moyo wako bado unawaendea wao, sifa zao, hadhi zao, na ushawishi wao. Ilhali unazidi kuchukua mtazamo ambapo unaona kazi ya Kristo kuwa ngumu sana kukubali na huko tayari kuikubali. Hii ndiyo maana Ninasema hauna imani ya kumkubali Kristo. Sababu iliyokufanya Umfuata mpaka leo hii ni kuwa hukuwa na chaguo jingine. Moyoni mwako milele mna picha nyingi refu; huwezi kusahau kila neno lao na matendo yao, au maneno yao ya ushawishi na mikono. Wao ni, katika moyo wenu, wakuu milele na tena mashujaa milele. Lakini hivi sivyo ilivyo na Kristo wa leo hii. Yeye moyoni mwako kamwe Hana umuhimu na kamwe Hastahili heshima. Kwa maana Yeye ni wa kawaida sana, mwenye ushawishi mdogo zaidi na Yuko mbali na ukuu.

Kwa vyovyote vile, Ninasema kuwa wote wale wasioenzi ukweli ni wasioamini na waasi wa ukweli. Watu kama hawa hawatawahi kuipokea idhini ya Kristo. Umeweza sasa kutambua kiasi cha kutoamini kilicho ndani yako? Na kiasi gani cha usaliti kwa Kristo? Kwa hivyo Nakuhimiza hivi; Kwa maana umeichagua njia ya ukweli, basi huna budi ila kujitolea na moyo wote; usiwe na kuchanganyikiwa au wa kusitasita. Unafaa kufahamu kuwa Mungu si wa ulimwengu huu au wa mtu yeyote, bali ni wa wale wote wanaoamini katika Mungu kwa kweli, wote wale wanaomwabudu, na wote wale waliojitolea na wanaoamini katika Mungu.

Kwa wakati huu, kuna kutoamini kwingi sana ndani yenu. Jaribu kuangalia kwa makini ndani yako na kwa hakika mtajionea jibu mwenyewe. Unapopata jibu halisi, basi utakubali kuwa wewe kweli si muumini wa Mungu, bali ni mdanganyifu, unayekufuru, unayemsaliti, na usiye mwaminifu kwa Mungu. Kisha utagundua kuwa Kristo si mwanadamu, ila ni Mungu. Siku hiyo itakapowadia, basi utamheshimu, utamcha na utampenda kwa dhati Kristo. Kwa sasa, imani yenu ni asilimia thelathini tu ya moyo wenu, ilhali asilimia sabini zimekumbwa na shaka. Tendo lolote likifanywa na sentensi yoyote ikitamkwa na Kristo vyaweza kusababisha muwe na fikira na maoni kumhusu Yeye. Fikira na maoni haya hutokana na kutokuwa na imani kabisa ndani Yake. Mnamtamani na kumcha tu Mungu msiyemwona aliye mbinguni lakini hauna haja na Kristo Anayeishi duniani. Hii pia si ni ukosefu wa imani? Mnamtamani tu Mungu Aliyefanya kazi kitambo kile lakini hutaki kukumbana na Kristo wa leo. Hizi ndizo huwa “imani” zilizochanganyika katika mioyo yenu isiyomwamini Kristo wa leo. Sikuchukulii kwa hali ya chini kwa maana ndani yako mna kutoamini kwingi, ndani yenu mna uchafu mwingi sana ambao lazima uchunguzwe kwa kina. Madoa na uchafu huu ni ishara kuwa huna imani hata kidogo; ni alama za ninyi kumkana Kristo na huonyesha kuwa nyinyi ni msaliti wa Kristo. Hiyo ni kama kitambaa kinachofunika ufahamu wenu wa Kristo, kizuizi cha nyinyi kupatwa na Kristo, kitu kinachowakinga kulingana na Kristo, na dhihirisho kuwa Kristo Hawatambui. Huu ndio wakati wa kuchunguza kila sehemu ya maisha yenu! Kufanya hivyo kutakufaidi kwa njia zote ambazo mnaweza kufikiria!

Kristo Hufanya Kazi ya Hukumu kwa Ukweli

Kazi ya siku za mwisho ni kutenganisha vitu vyote kulingana na jinsi yavyo, kuhitimisha mpango wa usimamizi wa Mungu, kwa maana muda u karibu na siku ya Mungu imewadia. Mungu huwaleta wote ambao wameingia katika ufalme Wake, yaani, wale wote ambao wamekuwa waaminifu Kwake mpaka mwisho, katika enzi ya Mungu Mwenyewe. Hata hivyo, kabla ya kuja kwa enzi ya Mungu Mwenyewe, kazi Atakayofanya Mungu si kutazama matendo ya mwanadamu wala kuchunguza maisha ya wanadamu, ila ni kuhukumu uasi wake, kwa maana Mungu atawatakasa wale wote wanaokuja mbele ya kiti Chake cha enzi. Wale wote ambao wamefuata nyayo za Mungu mpaka siku hii ni wale ambao wamekuja mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, na kwa hivyo, watu wote wanaokubali kazi ya Mungu katika awamu yake ya mwisho ni chombo cha utakaso wa Mungu. Kwa maneno mengine, wale wote wanaoikubali kazi ya Mungu katika awamu yake ya mwisho ni chombo cha hukumu ya Mungu.

“Hukumu” katika maneno yaliyonenwa awali—hukumu itanza na nyumba ya Mungu—inarejelea hukumu ambayo Mungu anatoa leo kwa wale wanaokuja mbele ya kiti Chake cha enzi katika siku za mwisho. Pengine kuna wale wanaoamini katika mawazo ya kimiujiza kama yale, siku za mwisho zitakapowadia, Mungu ataandaa meza kubwa mbinguni, ambako kitambaa cheupe kitatandikwa, kisha, Mungu ataketi kwenye kiti kikuu cha enzi na wanadamu wote wakipiga magoti ardhini, Atafichua dhambi za kila mwanadamu na hivyo kubainisha iwapo atapaa juu mbinguni ama atakupwa chini kwenye ziwa la moto wa jehanamu. Haijalishi mawazo ya mwanadamu yalivyo, kiini cha kazi ya Mungu hakiwezi kubadilishwa. Mawazo ya mwanadamu ni miundo ya fikra za mwanadamu tu na yanatoka kwenye ubongo wa mwanadamu, na yametungwa na kuunganishwa kutokana na mambo aliyoyaona na kuyasikia. Kwa hivyo Nasema, kwa vyovyote vile hata picha zilizowazwa ziwe za hali ya juu kiasi gani, bado ni kama mchoro tu na haziwezi kubadilishwa na mpango wa kazi ya Mungu. Hata hivyo, mwanadamu amepotoshwa na Shetani, sasa ataweza kuyaelewa mawazo ya Mungu? Mwanadamu huiona kazi ya hukumu ya Mungu kuwa ya ajabu mno. Mwanadamu anaamini kwamba kwa sababu ni Mungu Mwenyewe anayefanya kazi ya kuhukumu, basi lazima iwe ni ya kiwango cha juu zaidi na isioeleweka kwa wanadamu wenye mwili wa kufa, na lazima inasikika katika mbingu yote na kutetemeshwa dunia; vinginevyo itakuwaje kazi ya hukumu ya Mungu? Mwanadamu anaamini kuwa, kwa maana hii ni kazi ya hukumu, basi lazima Mungu ni wa kuvutia na mwenye uadhama Anapofanya kazi, na wale wanaohukumiwa lazima wawe wanalia kwa sauti wakitoa machozi wakiwa kwenye magoti wakiomba msamaha. Onyesho hili lazima ni la kustaajabisha sana na la kuisisimua mno.... Kila mtu hudhani kazi ya hukumu ya Mungu kuwa ya miujiza. Je, unajua, hata hivyo, kwamba wakati ule Mungu alikuwa ameanza kazi Yake ya kuhukumu miongoni mwa wanadamu, wewe bado umebaki katika hali ya kutotambua? Kwamba, wakati ambao

unadhani kuwa kazi ya hukumu ya Mungu inaanza rasmi, tayari umewadia wakati ambapo Mungu kuzifanya upya mbingu na nchi? Wakati huo, pengine utakuwa tu umeelewa maana ya maisha, lakini kazi ya adhabu ya Mungu isiyo na huruma itakuleta kuzimu, ukiwa bado usingizini. Hapo tu ndipo kwa ghafla utafahamu kuwa kazi ya hukumu ya Mungu itakuwa imeshahitimika.

Tusipoteze muda wa thamani, na tusizungumzie tena mada hizi za kuchukiza na za karaha. Badala yake, tuzungumzie kinachofanyiza hukumu. Ikifika kwa neno “hukumu,” utawaza juu ya maneno ambayo Yehova alizungumza kila mahali na pia maneno ya kukaripia ambayo Yesu aliwaambia Mafarisayo. Ingawa maneno haya ni yenye ukali, sio hukumu ya Mungu kwa mwanadamu; maneno tu ambayo yamezungumzwa na Mungu katika mazingira tofauti, yaani, mandhari tofauti, maneno haya ni tofauti kabisa na yale maneno anayonena Kristo wakati Anamhukumu mwanadamu siku za mwisho. Katika siku za mwisho, Kristo anumia ukweli tofauti kumfunza mwanadamu, kufichua kiini cha mwanadamu, na kuchangua maneno na matendo yake. Maneno haya yanajumuisha ukweli mbalimbali, kama vile wajibu wa mwanadamu, jinsi mwanadamu anavyofaa kumtii Mungu, jinsi mwanadamu anavyopaswa kuwa mwaminifu kwa Mungu, jinsi mwanadamu anavyostahili kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu wa kawaida, na pia hekima na tabia ya Mungu, na kadhalika. Maneno haya yote yanalenga nafsi ya mwanadamu na tabia yake potovu. Hasa, maneno hayo yanayofichua vile mwanadamu humkataa Mungu kwa dharau yanazungumzwa kuhusiana na vile mwanadamu alivyo mfano halisi wa Shetani na nguvu ya adui dhidi ya Mungu. Mungu anapofanya kazi Yake ya hukumu, Haiweki wazi asili ya mwanadamu kwa maneno machache tu; Anafunua, kushughulikia na kupogoa kwa muda mrefu. Mbinu hizi za ufunuo, kushughulika, na kupogoa haziwezi kubadilishwa na maneno ya kawaida, ila kwa ukweli ambao mwanadamu hana hata kidogo. Mbinu kama hizi pekee ndizo huchukuliwa kama hukumu; ni kwa kupitia kwa hukumu ya aina hii pekee ndio mwanadamu anaweza kutiishwa na kushawishiwa kabisa kujisalimisha kwa Mungu, na zaidi ya hayo kupata ufahamu kamili wa Mungu. Kile ambacho kazi ya hukumu humletea mwanadamu ni ufahamu wa uso halisi wa Mungu na ukweli kuhusu uasi wake mwenyewe. Kazi ya hukumu humruhusu mwanadamu kupata ufahamu zaidi wa mapenzi ya Mungu, wa makusudi ya kazi ya Mungu, na wa mafumbo yasiyoweza kueleweka kwa mwanadamu. Pia inamruhusu mwanadamu kutambua na kujua asili yake potovu na asili ya upotovu wake, na pia kugundua ubaya wa mwanadamu. Matokeo haya yote huletwa na kazi ya hukumu, kwa maana asili ya kazi ya aina hii hasa ni kazi ya kuweka wazi ukweli, njia, na uhai wa Mungu kwa wale wote walio na imani ndani Mwake. Kazi hii ni kazi ya hukumu inayofanywa na Mungu. Usipouchukulia ukweli huu kuwa muhimu na kila mara kufikiria kuuepuka au kutafuta njia nyingine isipokuwa ukweli, basi ninasema kuwa wewe ni mtenda dhambi mkubwa. Iwapo una imani kwa Mungu, lakini hutafuti

ukweli au mapenzi ya Mungu, wala hupendi njia inayokuleta karibu na Mungu, basi nakwambia kuwa wewe ni yule anayejaribu kuepuka hukumu, na kwamba wewe ni kibaraka na msaliti anayekikimbia kiti kikuu cheupe cha enzi. Mungu hatawasamehe waasi wowote wanaotoroka machoni Pake. Wanadamu wa aina hii watapokea adhabu kali zaidi. Wale wanaokuja mbele za Mungu ili wahukumiwe, na zaidi ya hayo wametakaswa, wataishi milele katika ufalme wa Mungu. Bila shaka, hili ni jambo ambalo liko katika siku za usoni.

Kazi ya hukumu ni kazi ya Mungu Mwenyewe, kwa hivyo lazima ifanywe na Mungu Mwenyewe kwa kawaida; haiwezi kufanywa na mwanadamu kwa niaba Yake. Kwa sababu hukumu ni kumshinda mwanadamu kupitia ukweli, hakuna shaka kuwa Mungu bado Anaonekana kama kiumbe aliyepata mwili kufanya kazi hii miongoni mwa wanadamu. Hiyo ni kumaanisha, wakati wa siku za mwisho, Kristo atautumia ukweli kuwafunza wanadamu duniani kote na kufanya ukweli wote ujulikane kwao. Hii ni kazi ya hukumu ya Mungu. Wengi wana hisia mbaya kuhusu kupata mwili kwa Mungu kwa mara ya pili, kwa maana mwanadamu huona vigumu kuamini ya kwamba Mungu angefanya kazi ya hukumu akiwa na mwili. Hata hivyo, lazima Nikueleze kwamba mara nyingi kazi ya Mungu huzidi sana matarajio ya mwanadamu na ni vigumu kwa mawazo yao kukubali. Kwa maana wanadamu ni mabuu tu kwenye ardhi, ilhali Mungu ni mkuu Anayejaza ulimwengu mzima; mawazo ya mwanadamu ni kama shimo la maji machafu ambayo yanazalisha mabuu peke yake, ilhali kila hatua ya kazi inayoelekezwa na mawazo ya Mungu ni utoneshaji wa hekima ya Mungu. Mwanadamu hutaka kila wakati kushindana na Mungu, ambalo kwalo Nasema ni wazi nani atapata hasara mwishowe. Nawasihi nyote msijichukulie kuwa wa maana zaidi kushinda dhahabu. Ikiwa wengine wanaweza kukubali hukumu ya Mungu, ni kwa nini wewe usiikubali? Ni vipi ambavyo ninyi ni bora zaidi kuliko wengine? Iwapo wengine wanaweza kuinamisha vichwa vyao mbele ya ukweli, ni kwa nini usifanye vile pia? Mwelekeo mkuu wa kazi ya Mungu hauwezi kukomeshwa. Hatarudia kazi ya hukumu tena kwa sababu tu ya “mchango” ambao umetoa, na utajawa na majuto mengi kwa kupoteza nafasi nzuri kama hiyo. Usipoyaamini maneno Yangu, basi kingoje tu kiti cheupe kikuu cha enzi kilicho angani kipitisha hukumu juu yako! Lazima ujue kwamba Waisraeli wote walimkataa kwa dharau na kumkana Yesu, ilhali uhakika wa ukombozi wa Yesu kwa wanadamu ulizidi kusambazwa kote ulimwenguni hadi miisho ya dunia. Je, hili silo jambo ambalo Mungu tayari Amelitimiza? Iwapo bado unangoja Yesu aje kukupeleka mbinguni, basi Nasema kuwa wewe ni kipande sugu cha mti mkavu^[a]. Yesu hatamkubali mfuasi bandia kama wewe asiye mwaminifu kwa ukweli na anayetafuta baraka pekee. Hasha, Hataonyesha huruma Anapokutupa kwenye ziwa la moto uungue kwa makumi ya maelfu ya miaka.

Je, sasa unaelewa hukumu ni nini na ukweli ni nini? Ikiwa umeelewa, basi Nakusihi ujisalimishe kwa hukumu kwa utii, la sivyo hutapata kamwe fursa ya kusifiwa na Mungu au

kupelekwa na Mungu katika ufalme Wake. Wale wanaokubali hukumu pekee yake na hawawezi kamwe kutakaswa, yaani, wale wanaotoroka wakati kazi ya hukumu inapoendelea, watachukiwa na kukataliwa na Mungu milele. Dhambi zao ni nyingi zaidi, na za kusikitisha zaidi, kuliko zile za Mafarisayo, kwa maana wamemsaliti Mungu na ni waasi dhidi ya Mungu. Wanadamu wa aina hii wasiostahili hata kufanya huduma watapokea adhabu kali zaidi, aidha adhabu inayodumu milele. Mungu hatamsamehe msaliti yeyote ambaye kwa wakati mmoja alidhihirisha uaminifu kwa Mungu kwa maneno tu ilhali alimsaliti Mungu. Wanadamu kama hao watapata adhabu ya malipo kupitia adhabu ya roho, nafsi, na mwili. Je, huu si ufichuzi wa tabia yenye haki ya Mungu? Je, hili silo kusudi la Mungu katika kumhukumu mwanadamu na kumfichua mwanadamu? Wakati wa hukumu, Mungu huwapeleka wote wanaofanya aina zote za uovu mahali palipojaa roho waovu, Akiacha miili yao ya nyama iharibiwe vile wapendavyo roho hao waovu. Miili yao inatoa harufu mbaya ya maiti, na adhabu kama hiyo ndiyo inayowafaa. Mungu huandika kwenye vitabu vyao vya kumbukumbu kila mojawapo ya dhambi za waumini hawa wanafiki wasio waaminifu, mitume wanafiki, na wafanyakazi bandia; kisha, wakati unapowadia, Anawatupa katikati ya roho wachafu, Akiacha miili yao ichafuliwe na roho hao wachafu wanavyopenda, na matokeo yake ni kwamba hawatawahi kamwe kuzaliwa upya katika miili mipya na hawatauona mwanga kamwe. Wale wanafiki waliotoa huduma wakati mmoja lakini hawawezi kuwa waaminifu mpaka mwisho wanahesabiwa na Mungu miongoni mwa waovu, ili watembe katika baraza la waovu, na kuungana na halaiki ya wasio na mpangilio; mwishowe, Mungu atawaangamiza. Mungu huwatenga na Hawatambui wote ambao hawajawahi kuwa waaminifu kwa Kristo au kuweka juhudi yoyote, na Atawaangamiza wote wakati wa mabadiliko ya enzi. Hawatakuwepo tena duniani, sembuse kupata njia ya kuingia katika ufalme wa Mungu. Wale ambao hawajawahi kuwa wa kweli kwa Mungu lakini wamelazimishwa na hali kumshughulikia Mungu kwa uzembe wanahesabiwa miongoni mwa wale wanaotoa huduma kwa watu wa Mungu. Ni idadi ndogo tu ya wanadamu wa aina hii ndio wanaweza kuendelea kuishi, huku wengi wao wataangamia pamoja na wasiohitimu hata kufanya huduma. Hatimaye, Mungu ataleta kwenye ufalme Wake wale wote walio na mawazo kama Yake, watu na wana wa Mungu na vilevile waliojaaliwa na Mungu kuwa makuhani. Hili ndilo tone Analopata Mungu kutokana na kazi Yake. Na kwa wale wasio katika sehemu zozote zilizotengwa na Mungu, watahesabiwa miongoni mwa wasioamini. Na kwa hakika mnaweza kuwaza jinsi hatima yao itakavyokuwa. Tayari Nimewaambia yote Ninayopaswa kusema; njia mnayochagua itakuwa uamuzi wenu kufanya. Mnachopaswa kuelewa ni hiki: Kazi ya Mungu kamwe haimsubiri yeyote asiyeweza kwenda sambamba na Mungu, na tabia ya Mungu ya haki haimwonyeshi mwanadamu yeyote huruma.

Tanbihi:

a. Kipande cha mti mkavu: nahau ya Kichina inayomaanisha “hali isiyo na matumaini.”

Je, Ulikuwa Unajua? Mungu Amefanya Jambo Kubwa Miongoni Mwa Wanadamu

Enzi ya zama ishaenda, na enzi mpya imefika. Mwaka baada ya mwaka na siku baada ya siku, Mungu amefanya kazi nyingi. Alikuwa duniani, kisha Akaondoka. Mzunguko kama huu umeendelea kwa vizazi vingi. Siku ya leo, Mungu anaendelea kama mbeleni kufanya kazi Anayopaswa kufanya, kazi ambayo bado Hajaikamilisha, kwani hadi leo, bado Hajaingia mapumzikoni. Kutoka wakati wa uumbaji hadi leo, Mungu amefanya kazi nyingi, lakini ulijua kwamba kazi anayoifanya Mungu leo ni nyingi kuliko awali na kipimo ni kikubwa zaidi? Hii ndiyo maana Nasema Mungu amefanya jambo kubwa miongoni mwa wanadamu. Kazi zote za Mungu ni muhimu sana, iwe kwa mwanadamu ama Mungu, kwani kila kitu cha kazi Yake kina uhusiano na mwanadamu.

Sababu kazi ya Mungu haiwezi kuonekana wala kuguswa, sembuse kuonwa na ulimwengu, basi jinsi gani ikawa kitu kikubwa? Ni jambo la aina gani linachukuliwa kuwa kubwa? Hakika hakuna anayeweza kukataa kuwa kazi zote za Mungu zinaweza kuchukuliwa kuwa kubwa, lakini mbona Nasema kazi anayofanya Mungu leo iko hivi? Ninaposema kwamba Mungu amefanya kitu kikubwa, hii bila shaka inahusisha siri nyingi ambazo mwanadamu bado hajazielewa. Wacha tuzizungumzie sasa.

Yesu alizaliwa horini wakati ambao hungevumilia kuwepo Kwake, lakini dunia bado haingemzuia, na Aliishi miongoni mwa wanadamu kwa miaka thelathini na tatu chini ya ulinzi wa Mungu. Kwa miaka hiyo yote ya maisha, Alikuwa na uzoefu wa uchungu wa dunia na Akaonja maisha ya taabu duniani. Alilichukua jukumu zito la kusulubiwa ili kuwakomboa wanadamu wote. Aliwakomboa wote wenye dhambi walioishi chini ya miliki ya Shetani, na mwishowe, mwili Wake uliofufuka ukarudi mahali Pake pa mapumziko. Sasa kazi mpya ya Mungu imeanza, na pia ni mwanzo wa enzi mpya. Mungu analeta nyumbani Kwake wale waliokombolewa kuanza kazi Yake ya wokovu. Wakati huu, kazi ya wokovu ni ya kina kuliko nyakati za nyuma. Haitafanywa na Roho Mtakatifu akifanya kazi ndani ya mwanadamu ili kumruhusu kubadilika mwenyewe, wala haitafanywa kupitia mwili wa Yesu akijitokeza miongoni mwa wanadamu, na sembuse haitafanywa kwa namna ingine. Badala yake, kazi itafanywa na kuongozwa na Mungu mwenye mwili Mwenyewe. Hii inafanywa ili kumwongoza binadamu katika kazi mpya. Hili si jambo zuri? Mungu hafanyi kazi hii kupitia sehemu ya wanadamu ama kupitia unabii, lakini kwa Mungu Mwenyewe. Wengine wanaweza kusema kuwa hili si jambo kubwa na kwamba haliwezi kumletea mwanadamu furaha mno. Hata hivyo, Nitakuambia kwamba kazi ya Mungu siyo tu hii, ila kitu kikubwa zaidi na kingi zaidi.

Wakati huu, Mungu haji kufanya kazi kwa mwili wa kiroho ila kwa ule wa kawaida sana. Sio tu mwili wa kupata mwili kwa Mungu kwa mara ya pili, lakini pia mwili ambao Mungu anarudia. Ni mwili wa kawaida sana. Ndani Yake, huwezi kuona chochote kilicho tofauti na cha wengine, lakini unaweza kupokea kutoka Kwake ukweli ambao hujawahi kusikia mbeleni. Mwili huu usio na umuhimu ni mfano halisi wa maneno yote ya kweli kutoka kwa Mungu, ambao hufanya kazi ya Mungu siku za mwisho, na maonyesho ya tabia nzima ya Mungu kwa mwanadamu kuja kujua. Je, hukutamani sana kumwona Mungu aliye mbinguni? Je, hutamani sana kumwelewa Mungu aliye mbinguni? Je, hutamani sana kuona hatima ya mwanadamu? Atakueleza hizi siri zote ambazo hakuna mwanadamu ameweza kukuambia, na pia Atakuelezea kuhusu ukweli usioelewa. Yeye ndiye lango la kuingia katika ufalme, na mwongozo wako katika enzi mpya. Mwili wa kawaida kama huu una siri nyingi zisizoeleweka. Matendo Yake labda hayaeleweki kwako, lakini lengo la kazi yote Anayoifanya limekutosha kuona kuwa Yeye si mwili wa kawaida anavyoamini mwanadamu. Kwani Anawakilisha mapenzi ya Mungu na pia utunzaji anaonyesha Mungu kwa mwanadamu siku za mwisho. Ingawa huwezi kuyasikia maneno Anayozungumza yanayoonekana kutingisha mbingu na dunia wala kuona macho Yake kama moto mkali, na ingawa huwezi kuhisi nidhamu ya fimbo Yake ya chuma, unaweza kusikia kupitia maneno Yake ghadhabu ya Mungu na kujua kwamba Mungu Anaonyesha huruma kwa mwanadamu; unaweza kuona tabia ya haki ya Mungu na hekima Yake, na zaidi ya hayo, kutambua wasiwasi na utunzaji anao Mungu kwa wanadamu wote. Kazi ya Mungu ya siku za mwisho ni kuruhusu mwanadamu kumwona Mungu aliye mbinguni Akiishi miongoni mwa wanadamu duniani, na kumwezesha mwanadamu kuja kumjua, kumtii, kumheshimu, na kumpenda Mungu. Hii ndiyo maana Amerudi kwa mwili kwa mara ya pili. Ingawa kile anachokiona mwanadamu siku hii ni Mungu aliye sawa na mwanadamu, Mungu aliye na pua na macho mawili, na Mungu asiye wa ajabu, mwishowe, Mungu atawaonyesha kwamba bila kuwepo kwa huyu mwanadamu, mbingu na dunia zitapitia mabadiliko makuu; bila kuwepo kwa huyu mwanadamu, mbingu itapungukiwa na mwangaza, dunia itakuwa vurugu, na wanadamu wote wataishi katika njaa na mabaa. Atawaonyesha kuwa bila wokovu wa Mungu mwenye mwili katika siku za mwisho, basi Mungu Angekuwa Ashawaangamiza wanadamu wote kuzimu kitambo sana; bila kuwepo kwa mwili huu, basi daima mngekuwa viongozi wa wenye dhambi na maiti milele. Mnapaswa kujua kwamba bila kuwepo kwa mwili huu, wanadamu wote wangetazamia msiba usioepukika na kupata kuwa ngumu kuponyoka adhabu kali zaidi ya Mungu katika siku za mwisho. Bila kuzaliwa kwa mwili huu wa kawaida, nyinyi nyote mngekuwa katika hali ambayo uhai wala kifo havitakuja bila kujali jinsi mtakavyovitafuta; bila kuwepo kwa mwili huu, basi siku hii hamngeweza kupokea ukweli na kuja mbele ya kiti cha Mungu cha enzi. Badala yake, mngedhibiwa na Mungu kwa sababu ya dhambi zenu zinazohuzunisha. Je, mnajua? Kama sio kwa kurudi kwa Mungu kwa mwili, hakuna ambaye

angepata nafasi ya wokovu; na isipokuwa kwa kuja kwa mwili huu, Mungu angekuwa ameimaliza kitambo enzi ya zamani. Hivyo basi, mnaweza bado kuukataa kupata mwili kwa mara ya pili kwa Mungu? Sababu mnaweza kufaidika sana kutoka kwa huyu mwanadamu wa kawaida, basi mbona hamumkubali kwa urahisi?

Kazi ya Mungu ni ile usiyoweza kuelewa. Kama huwezi kufahamu kama uamuzi wako ni sahihi wala kujua kama kazi ya Mungu inaweza kufaulu, basi mbona usijaribu bahati yako na kuona iwapo huyu mwanadamu wa kawaida ni wa msaada mkubwa kwako, na iwapo Mungu amefanya kazi kubwa. Hata hivyo, lazima Nikuelezee kuwa wakati wa Nuhu, wanadamu walikuwa wamekula na kunywa, wakifunga ndoa na kupeana katika ndoa hadi kiwango ambacho Mungu asingevumilia kushuhudia, hivyo, Alituma chini mafuriko makubwa kuangamiza wanadamu na kuacha tu nyuma familia ya Nuhu ya watu wanane na aina yote ya ndege na wanyama. Katika siku za mwisho, hata hivyo, wale waliohifadhiwa na Mungu ni wale wote ambao wamekuwa waaminifu Kwake hadi mwisho. Ingawa nyakati zote mbili zilikuwa za upotovu mkubwa Asizoweza kuvumilia kushuhudia Mungu, na mwanadamu katika enzi zote mbili alikuwa mpotovu kiasi cha kumkana Mungu kama Bwana, watu wote katika wakati wa Nuhu waliangamizwa na Mungu. Mwanadamu katika enzi zote mbili amemhuzunisha Mungu sana, lakini Mungu bado Amebakia mvumilivu na wanadamu katika siku za mwisho hadi sasa. Mbona hivi? Hamjawahi kufikiria haya? Kama kweli hamjui, basi wacha Niwaelezee. Sababu Mungu anaweza kushughulika na wanadamu kwa neema siku za mwisho si kwamba ni wapotovu kidogo zaidi kuliko wanadamu katika wakati wa Nuhu ama kwamba wamemwonyesha Mungu toba, sembuse si kwamba Mungu hawezi kuvumilia kuwaangamiza wanadamu katika siku za mwisho ambapo teknolojia imeendelea. Badala yake, ni kwamba Mungu ana kazi ya kufanya kwa kundi la wanadamu katika siku za mwisho na hii itafanywa na Mungu mwenye mwili Mwenyewe. Zaidi ya hayo, Mungu atachagua sehemu ya kundi hili kama vyombo Vyake vya wokovu, tunda la mpango Wake wa usimamizi, na kuleta wanadamu kama hawa naye katika enzi ifuatayo. Kwa hivyo, bila kujali, hii gharama iliyolipwa na Mungu yote imekuwa katika maandalizi ya kazi ya kupata mwili Kwake katika siku za mwisho. Ukweli kwamba mmefika siku ya leo ni kwa sababu ya huu mwili. Ni kwa sababu Mungu huishi ndani ya mwili ndiyo mna nafasi ya kuishi. Hii bahati yote nzuri imepatwa kwa sababu ya huyu mwanadamu wa kawaida. Siyo haya tu, lakini mwishowe kila taifa litamwabudu huyu mwanadamu wa kawaida, na pia kumpa shukrani na kumtii huyu mwanadamu asiye muhimu, kwa sababu ni ukweli, uzima, na njia Aliyoleta ndivyo vilivyowaokoa wanadamu wote, kutuliza migogoro kati ya mwanadamu na Mungu, ikafupisha umbali kati yao, na kufungua kiungo kati ya mawazo ya Mungu na mwanadamu. Pia ni Yeye ambaye Ameleta hata utukufu zaidi kwa Mungu. Mwanadamu wa kawaida kama huyu hastahili uaminifu na ibada yako? Mwili wa

kawaida kama huu haufai kuitwa Kristo? Mwanadamu wa kawaida kama huyu hawezi kuwa maonyesho ya Mungu miongoni mwa wanadamu? Mwanadamu kama huyu anayesaidia wanadamu kuepuka maafa hastahili mapenzi yenu na nyinyi kumshikilia? Mkiukataa ukweli unaotamkwa kutoka mdomo Wake na pia kuchukia kuwepo Kwake miongoni mwenu, basi nini itakuwa majaliwa yenu?

Kazi yote ya Mungu katika siku za mwisho inafanywa kupitia huyu mwanadamu wa kawaida. Atakupa kila kitu, na juu ya hayo, Anaweza kuamua kila kitu kukuhusu. Mtu kama huyu anaweza kuwa mnavyoamini: mtu wa kawaida sana kiasi cha kutostahili kutajwa? Ukweli Wake hujatosha kuwashawishi kabisa? Ushuhuda wa vitendo Vyake hujatosha kuwashawishi kabisa? Ama ni kuwa njia Anayowaongozea haistahili nyinyi kuifuata? Ni nini kinachowasababisha kumchukia na kumtupilia mbali na kumwepuka? Ni Yeye anayeonyesha ukweli, ni Yeye anayetoa ukweli, na ni Yeye anayewawezesha kuwa na njia ya kusafiri. Inaweza kuwa kwamba bado hamwezi pata chembe cha kazi ya Mungu ndani ya ukweli huu? Bila kazi ya Yesu, mwanadamu hangeweza kushuka chini kutoka msalabani, lakini bila kupata mwili siku hii, wale wanaoshuka chini kutoka msalabani hawangewahi kusifiwa na Mungu ama kuingia katika enzi mpya. Bila kuja kwa huyu mwanadamu wa kawaida, basi hamngeweza kuwa na hii fursa ama kustahiki kuona uso wa ukweli wa Mungu, kwani nyinyi nyote ni wale ambao wangepaswa kuangamizwa kitambo sana. Kwa sababu ya kuja kwa Mungu mwenye mwili kwa mara ya pili, Mungu amewasamehe na kuwaonyesha huruma. Bila kujali, maneno ambayo lazima Niwaachie mwishowe ni haya: Huyu mwanadamu wa kawaida, ambaye ni Mungu mwenye mwili, ni wa umuhimu sana kwenu. Hili ndilo jambo kubwa ambalo Mungu tayari Amefanya miongoni mwa wanadamu.

Ni Kristo wa Siku za Mwisho Pekee Ndiye Anayeweza Kumpa Mwanadamu Njia ya Uzima wa Milele

Njia ya maisha si kitu ambacho mtu yeyote anaweza kumiliki, wala si kitu ambacho mtu yeyote anaweza kufikia kwa urahisi. Hii ni kwa sababu maisha yanaweza kuja tu kutoka kwa Mungu, ambayo ni kusema, Mungu Mwenyewe tu ndiye Anamiliki mali ya maisha, hakuna njia ya maisha bila Mungu Mwenyewe, na hivyo Mungu tu ndiye chanzo cha uzima, na kijito cha maji ya uzima kinachotiririka nyakati zote. Kutoka Alipoumba dunia, Mungu amefanya kazi kubwa inayoshirikisha uhai wa maisha, Amefanya kazi kubwa ambayo huletea mwanadamu maisha, na Amelipa gharama kubwa ili mtu aweze kupata uzima, kwa kuwa Mungu Mwenyewe ni uzima wa milele, na Mungu Mwenyewe ni njia ambayo kwayo mtu hufufuliwa. Mungu kamwe hajawahi kosa kwa moyo wa mwanadamu, na Anaishi miongoni mwa binadamu wakati wote. Amekuwa nguvu ya kuendesha maisha ya mwanadamu, chanzo cha kuwepo kwa

binadamu, na amana ya fahari ya kuwepo kwa binadamu baada ya kuzaliwa. Husababisha binadamu kuzaliwa upya, na kumwezesha kwa ushupavu kuishi kwa kila jukumu lake. Kwa sababu ya uwezo Wake, na nguvu ya maisha Yake yasiyopungua, binadamu ameishi kwa kizazi baada ya kizazi, ambapo nguvu ya uhai wa Mungu umekuwa uti wa mgongo wa kuwepo kwa binadamu, na ambayo Mungu amelipia gharama ambayo hakuna mtu wa kawaida amewahi kulipa. Nguvu za Mungu za maisha zinaweza kutawala juu ya nguvu zozote; zaidi ya hayo, inazidi mamlaka yoyote. Maisha Yake ni ya milele, nguvu zake za ajabu, na nguvu Zake za maisha haziwezi kuzidiwa na kiumbe yeyote au nguvu za adui. Nguvu za maisha ya Mungu zipo, na hung'aa mwangaza wake ulio mzuri sana, bila ya kujali muda au mahali. Mbingu na dunia zinaweza kupitia mabadiliko makubwa, lakini uzima wa Mungu ni ule ule daima. Mambo yote hupita, lakini maisha ya Mungu hubaki, kwa maana Mungu ni chanzo cha kuwepo kwa mambo yote, na mizizi ya kuwepo kwao. Asili ya maisha ya mwanadamu hutoka kwa Mungu, kuwepo kwa mbingu ni kwa sababu ya Mungu, na kuwepo kwa ardhi kunatokana na nguvu ya uhai wa Mungu. Hakuna kitu kinachomiliki nguvu kinachoweza kuzidi ukuu wa Mungu, na hakuna kitu chenye nguvu kinachoweza kuvunja mipaka ya mamlaka ya Mungu. Kwa njia hii, bila kujali wao ni nani, kila mtu lazima ajiwasilishe kwa utawala wa Mungu, kila mtu lazima aishi chini ya amri za Mungu, na hakuna mtu anayeweza kutoroka kutoka katika utawala Wake.

Pengine, sasa, unataka kupokea maisha, au labda unataka kupata ukweli. Vyovyote vilivyo, unataka kumpata Mungu, kumpata Mungu unayeweza kutegemea, na ambaye anaweza kukupa uzima wa milele. Ukitaka kupata uzima wa milele, lazima kwanza uelewe chanzo cha uzima wa milele, na lazima kwanza ujue Mungu yuko wapi. Tayari nilishasema Mungu pekee ndiye maisha yasiyobadilika, na Mungu tu ndiye aliye na njia ya maisha. Kwa kuwa maisha Yake ni imara, hivyo ni ya milele; kwa kuwa Mungu tu ndiye njia ya maisha, basi Mungu Mwenyewe ni njia ya uzima wa milele. Kwa hivyo, lazima kwanza uelewe aliko Mungu, na jinsi ya kupata njia hii ya uzima wa milele. Hebu sasa tushiriki kwa masuala haya mawili tofauti.

Kama kweli unataka kupata njia ya uzima wa milele, na kama wewe unayo tamaa katika utafutaji wako kwa ajili yake, basi kwanza ulijibu swali hili: Mungu yuko wapi leo? Labda utajibu kwamba Mungu anaishi mbinguni, bila shaka—Hangeishi katika nyumba yako? Labda unaweza kusema, kawaida Mungu anaishi kati ya mambo yote. Au unaweza kusema kwamba Mungu anaishi katika moyo wa kila mtu, au kwamba Mungu yuko katika ulimwengu wa kiroho. Mimi sipingi lolote kati ya haya, lakini lazima nifanue suala hilo. Sio sahihi kabisa kusema kwamba Mungu anaishi katika moyo wa mwanadamu, wala si makosa kabisa. Hiyo ni kwa sababu, miongoni mwa waumini katika Mungu, kuna wale ambao imani yao ni ya kweli na wale ambao imani yao ni uongo, kuna wale ambao Mungu anawakubali na wale ambao hawakubali, kuna wale ambao humfurahisha na wale ambao ni chukizo, na kuna wale ambao Yeye

huwafanya kamili na wale ambao hupunguza. Na hivyo Mimi Nasema kwamba Mungu Anaishi tu katika nyoyo za watu wachache, na watu hawa bila shaka ni wale ambao kweli wanaamini katika Mungu, wale ambao Mungu anawakubali, wale ambao humpendeza, na wale ambao Yeye huwafanya kamili. Wao ni wale wanaoongozwa na Mungu. Kwa kuwa wanaongozwa na Mungu, kwa hivyo ni watu ambao tayari wamesikia na kuona njia ya Mungu ya uzima wa milele. Wale ambao imani yao kwa Mungu ni ya uongo, wale ambao hawajaidhinishwa na Mungu, wale ambao wanadharauliwa na Mungu, wale ambao wamechujwa na Mungu—wamefungwa katika kukataliwa na Mungu, wamefungwa kubaki bila njia ya maisha, na wamefungwa kubaki wajinga wa kujua aliko Mungu. Kwa upande mwingine, wale ambao Mungu anaishi katika nyoyo zao wanajua aliko Mungu. Wao ni watu wale ambao Mungu huwapa njia ya uzima wa milele, na ni wale wanaomfuata Mungu. Je, unajua, sasa, aliko Mungu? Mungu yupo katika moyo wa mtu na upande wa mtu. Hayupo tu katika ulimwengu wa kiroho, na juu ya mambo yote, lakini hata zaidi Yupo duniani ambapo mwanadamu huishi. Na hivyo kufika kwa siku za mwisho kumechukua hatua ya kazi ya Mungu katika sehemu mpya. Mungu ana ukuu juu ya mambo yote katika ulimwengu, na Yeye ni uti wa mgongo wa mwanadamu katika moyo wake, na zaidi ya hayo, Yeye yuko miongoni mwa wanadamu. Ni kwa njia hii pekee Anaweza kuleta njia ya maisha kwa binadamu, na kumleta mwanadamu katika njia ya maisha. Mungu amekuja duniani, na Anaishi kati ya wanadamu, ili wanadamu wanaweza kupata njia ya maisha, na hivyo binadamu anaweza kuwepo. Wakati huo huo, Mungu pia huamuru mambo yote katika ulimwengu, ili wapate kushirikiana na usimamizi Wake miongoni mwa wanadamu. Na hivyo, kama wewe unakiri tu kwamba Mungu yuko mbinguni na katika moyo wa mwanadamu, lakini usikiri ukweli wa kuwepo kwa Mungu miongoni mwa watu, basi kamwe hutapata uzima, na kamwe hutapata njia ya kweli.

Mungu Mwenyewe ni maisha, na kweli, na uzima Wake na ukweli hutawala. Wale ambao hawana uwezo wa kupata ukweli kamwe hawatapata uzima. Bila mwongozo, msaada, na utoaji wa kweli, nanyi tu mtapata barua, mafundisho, na zaidi sana, kifo. Maisha ya Mungu ni ya milele, na ukweli wake na maisha hupatana. Kama huwezi kupata chanzo cha ukweli, basi huwezi kupata lishe ya maisha; kama huwezi kupata starehe ya maisha, basi utakuwa hakika huna ukweli, na hivyo mbali na mawazo na dhana, ukamilifu wa mwili wako hautakuwa chochote ila mwili, mwili wako unaonuka. Ujue kwamba maneno ya vitabu hayaahasabiki kama maisha, kumbukumbu za historia haziwezi kupokelewa kama ukweli, na mafundisho ya siku za nyuma hayawezi kutumika kama sababu ya maneno ya sasa anayosema Mungu.

Kinachoonyeshwa tu na Mungu anapokuja duniani na kuishi miongoni mwa binadamu ni ukweli, maisha, mapenzi ya Mungu, na njia Yake ya sasa ya kufanya kazi. Kama wewe utatumia rekodi ya maneno yaliyosemwa na Mungu wakati wa enzi zilizopita leo, basi wewe ni mtafutaji wa

mambo ya kale, na njia bora ya kukueleza wewe ni mtaalamu wa urithi wa kihistoria. Kwa sababu wewe daima unaamini katika athari ya kazi ambayo Mungu alifanya katika nyakati zilizopita, amini tu katika kivuli cha Mungu alichowacha awali Alipokuwa Akifanya kazi miongoni mwa wanadamu, na kuamini tu kwa njia ambayo Mungu aliwapa wafuasi wake katika nyakati za zamani. Huamini katika mwelekeo wa kazi ya Mungu leo, huamini katika uso wa utukufu wa Mungu leo, na huamini katika njia ya sasa ya kweli iliyotolewa na Mungu. Na hivyo wewe ni mwotaji wa mchana ambaye hana ufahamu kamwe na hali ya mambo ya sasa. Kama sasa bado wewe unafuata maneno yasiyokuwa na uwezo wa kuleta maisha kwa binadamu, basi wewe ni kipande cha ukuni uliokauka kisicho na matumaini^[a], kwa maana wewe ni mwenye kushikilia ukale mno, asiyeweza kutiishwa kwa urahisi, huwezi kusikiza wosia!

Mungu aliyepata mwili Anaitwa Kristo, na hivyo Kristo ambaye Anaweza kuwapa binadamu ukweli anaitwa Mungu. Hakuna kitu kikuu kuliko hiki, kwa kuwa Anayo hali ya Mungu, na ana tabia za Mungu, na hekima katika kazi Yake, ambayo haiwezi kupatikana kwa binadamu. Wale wanaojiita Kristo, walakini hawawezi kufanya kazi ya Mungu, ni matapeli. Kristo sio tu udhihirisho wa Mungu duniani, bali pia, mwili hasa ulioigwa na Mungu kufanya na kutimiza kazi Yake kati ya wanadamu. Mwili huu si ule unaoweza kubadilishwa na mtu yeyote tu, lakini ambao unaweza kutosha kufanya kazi ya Mungu duniani, na kueleza tabia ya Mungu, na pia kumwakilisha Mungu, na kumpa binadamu maisha. Hivi karibuni au baadaye, wale wanaojifanya kuwa Kristo wataanguka wote, ingawa wanadai kuwa Kristo, hawana chochote cha hali ya Kristo. Na hivyo Mimi nasema kwamba hali halisi ya Kristo haiwezi kuelezwa na mwanadamu, bali inajibiwa na kuamuliwa na Mungu Mwenyewe. Kwa njia hii, kama kweli unataka kutafuta njia ya maisha, lazima kwanza ukiri kuwa ni kwa kuja duniani ndipo Anazirejesha njia za maisha kwa binadamu, na lazima kukiri ni katika siku za mwisho Yeye anakuja duniani kuhifadhi njia ya maisha kwa mwanadamu. Haya sio ya wakati wa nyuma; yanatendeka leo.

Kristo wa siku za mwisho huleta uzima, na huleta kudumu kwa njia ya kweli na ya milele. Ukweli huu ni njia ambayo kwayo binadamu atapata uzima, na njia pekee ambayo mtu atamjua Mungu na kuidhinishwa na Mungu. Kama hutatafuta njia ya maisha inayotolewa na Kristo wa siku za mwisho, basi kamwe hutapata kibali cha Yesu, na kamwe hutastahili kuingia lango la ufalme wa mbinguni, maana wewe ni kikaragosi na mfungwa wa historia. Wale ambao wanadhibitiwa na kanuni, na maandiko, na waliofungwa na historia kamwe hawataweza kupata maisha, na kamwe hawataweza kupata njia ya daima ya maisha. Hiyo ni kwa sababu yote walio nayo ni maji machafu ambayo yameshikiliwa kwa maelfu ya miaka badala ya maji ya uzima yanayotiririka kutoka kwenye kiti cha enzi. Wale ambao hawajaruzukiwa maji ya uzima daima watabakia maiti, vitu vya kuchezeza na Shetani, na wana wa Jehanamu. Je, basi jinsi gani

wanaweza kumtazama Mungu? Kama wewe kamwe hujaribu kushikilia kwenye siku zilizopita, jaribu tu kuweka mambo kama yalivyo kwa kusimama kwa utulivu, na wala hujaribu kubadili hali kama ilivyo na kuacha historia, basi wewe hutakuwa daima dhidi ya Mungu? Hatua za kazi ya Mungu ni kubwa na zenye nguvu, kama kufurika kwa mawimbi na mngurumo wa radi—ilhali wewe unakaa na kwa uvivu ukisubiri uharibifu, na kujikita katika upumbavu wako na kutofanya chochote. Kwa njia hii, jinsi gani unaweza kuchukuliwa kama mtu anayefuata nyayo za Mwanakondoo? Jinsi gani unaweza kuhalalisha Mungu unayeshikilia kama Mungu ambaye ni daima mpya na si kamwe wa zamani? Na jinsi gani maneno ya vitabu vyako vya manjano yanaweza kukubeba hadi enzi mpya? Yanawezaje kukuongoza katika kutafuta hatua za kazi ya Mungu? Na jinsi gani yanaweza kukuchukua wewe kwenda mbinguni? Unayoshikilia mikononi ni barua ambazo zisizoweza kukuondolea kitu ila furaha ya muda mfupi, sio ukweli unaoweza kukupa maisha. Maandiko unayosoma ni yale tu ambayo yanaweza kuimarisha ulimi wako, sio maneno ya hekima ambayo yanaweza kukusaidia kujua maisha ya binadamu, sembuse njia zinazoweza kukuongoza kuelekea kwa ukamilifu. Je, si tofauti hii hukupa sababu kwa ajili ya kutafakari? Je, si inakuruhusu kuelewa siri zilizomo ndani? Je, una uwezo wa kujiwasilisha mwenyewe mbinguni kukutana na Mungu? Bila kuja kwa Mungu, je, unaweza kujichukua mwenyewe kwenda mbinguni kufurahia pamoja na familia ya Mungu? Je, wewe bado unaota sasa? Basi, Napendekeza sasa acha kuota, na kuangalia Anayefanya kazi sasa, na Anayefanya kazi ya kuwaokoa binadamu siku za mwisho. Kama huwezi, wewe kamwe hutapata ukweli, na kamwe hutapata uzima.

Wale ambao wanataka kupata uzima bila kutegemea ukweli wa neno la Kristo ni watu wafidhuli mno duniani, na wale ambao hawawezi kukubali njia ya maisha inayoletwa na Kristo wamepotea ndotoni. Na hivyo nasema kwamba watu ambao hawakubali Kristo wa siku za mwisho watadharauliwa milele na Mungu. Kristo ni lango la binadamu kwa ufalme katika siku za mwisho, ambayo hakuna anayeweza kupita bila Yeye. Hakuna anayeweza kukamilishwa na Mungu ila kwa njia ya Kristo. Unaamini katika Mungu, na hivyo ni lazima ukubali neno Lake na kutii njia Yake. Lazima usifikiri juu ya kupata baraka tu bila kupokea ukweli, au kukubali utoaji wa maisha. Kristo Anakuja katika siku za mwisho ili wale wote ambao kweli wanaamini katika Yeye waweze kupata maisha. Kazi Yake ni kwa ajili ya kuhitimisha enzi ya zamani na kuingia enzi mpya, na ni njia ambayo lazima ichukuliwe na wale wote ambao wataingia enzi mpya. Kama huna uwezo wa kumtambua Yeye, na badala yake kumhukumu, kulikufuru jina Lake au hata kumtesa Yeye, basi wewe umefungwa kuchomwa milele, na kamwe hutaingia katika ufalme wa Mungu. Kwa maana Kristo Mwenyewe ni onyesho la Roho Mtakatifu, onyesho la Mungu, Yule ambaye Mungu amemkabidhi kufanya kazi Yake hapa duniani. Na hivyo nasema kwamba kama huwezi kukubali yote yanayofanywa na Kristo wa siku za mwisho, basi unakufuru Roho

Mtakatifu. Adhabu ambayo lazima ishuhudiwe na wale ambao wanakufuru Roho Mtakatifu ni hasa dhahiri kwa wote. Nawaambia tena kwamba kama mtampinga Kristo wa siku za mwisho, na kumkanusha, basi hakuna mtu ambaye anaweza kubeba matokeo ya hilo kwa niaba yako. Aidha, tangu siku hii na kuendelea huwezi kuwa na nafasi nyingine ya kupata kibali cha Mungu; hata kama utajaribu kujikomboa mwenyewe, kamwe tena hutautazama uso wa Mungu. Kwa kuwa unachopinga si binadamu, unachokataa si jambo dogo, bali ni Kristo. Je, unafahamu ghadhabu ya matokeo haya? Wewe hujafanya makosa madogo, bali umetenda uhalifu wa kutisha. Na hivyo Nashauri kila mtu kutoweka wazi meno yenu mbele ya ukweli, au kufanya shutuma bila ya kujali, kwa kuwa ni ukweli tu unaoweza kukuletea maisha, na hakuna kitu isipokuwa ukweli kinachoweza kukuruhusu kuzaliwa upya na kutazama uso wa Mungu.

Tanbihi:

a. Kipande cha gogo lililokufa: Nahau ya Kichina yenye maana “-siyoweza kusaidiwa.”

Tayarisha Matendo Mema ya Kutosha kwa ajili ya Hatima Yako

Nimefanya kazi nyingi miongoni mwenu na, bila shaka, Nimenena baadhi ya matamshi pia. Hata hivyo Sina budi kuhisi kwamba maneno Yangu na kazi Yangu havijatimiza lengo la kazi Yangu ya siku za mwisho kikamilifu. Maana katika siku za mwisho, kazi Yangu si kwa ajili ya mtu au watu fulani, bali ili kufafanua tabia Yangu ya asili. Hata hivyo, kutokana na sababu nyingi—pengine ukosefu wa muda au shughuli nyingi za kazi—watu hawajapata ufahamu wowote kunihusu kutokana na tabia Yangu. Kwa hivyo, Ninaanza mpango Wangu mpya, katika kazi Yangu ya mwisho, na kufungua ukurasa mpya katika kazi Yangu ili wale wanaoniona watajipiga kifuni na kulilia na kuombolezea bila kukoma kwa sababu ya uwepo Wangu. Hii ni kwa sababu Ninaleta mwisho wa wanadamu duniani, na kuanzia sasa na kuendelea, Ninaweka wazi tabia Yangu yote mbele ya wanadamu, ili wote wanijua na wale wote wasionijua waweze kuyafurahisha macho yao na kuona kwamba kweli, Nimekuja katika ulimwengu wa kibinadamu, Nimekuja duniani ambapo vitu vyote vinazidi kuongezeka. Huu ni mpango Wangu, na “kukiri” Kwangu kwa pekee tangu Niwaumbe wanadamu. Nawaomba mzingatie kwa makini kila Ninachokifanya, maana kiboko Changu kinawakaribia wanadamu tena, kwa wale wote wanaonipinga.

Pamoja na mbingu, Ninaanza kazi ambayo ni lazima Niifanye. Na kwa hiyo Ninapenya kati ya misururu ya watu na kupita kati ya mbingu na ardhi, bila ya yeyote kutambua miendo Yangu au kuyatambua maneno Yangu. Kwa hivyo, mpango Wangu unaendelea kusonga mbele kwa urahisi. Ni kwamba hisia zenu zote zimekufa ganzi kiasi kwamba hamtambui hatua za kazi

Yangu. Lakini kwa kweli siku moja itakuja ambapo mtatambua nia Zangu. Leo, Ninaishi pamoja nanyi, na Ninasumbuka pamoja nanyi, na kwa muda mrefu Nimekuja kuelewa mtazamo walio nao wanadamu kunielekea. Nisingependa kuzungumza zaidi kuhusu jambo hili, sembuse kutoa mifano zaidi ya suala hili linaloumiza. Natumai tu kwamba mtayakumbuka yale yote ambayo mmeyafanya, ili tuweze kulinganisha maelezo yetu siku tutakapokutana tena. Nisingependa kumshutumu yeyote miongoni mwenu kwa njia isiyo ya kweli, kwa sababu daima Nimekuwa Nikitenda kwa njia ya haki, bila upendeleo, na kwa heshima. Bila shaka, Natumai pia kwamba nyinyi mnaweza kuwa wazi waadilifu, na kutofanya lolote lililo kinyume na mbingu na ardhi na dhamiri yenu. Hili ndilo jambo la pekee Ninalowaomba mfanye. Watu wengi huhisi kusumbuka na kuona haya kwa sababu wametenda makosa mabaya, na wengi wanajionea aibu kwa sababu hawajawahi kutenda tendo lolote zuri. Tena wapo pia wengi ambao, mbali na kutahayari kwa ajili ya dhambi zao, wanakuwa wabaya zaidi, wakiitoa kabisa barakoa inayoficha sura zao mbaya—ambayo haikuwa bado imewekwa wazi kikamilifu—ili kujaribu tabia Yangu. Sijali, wala sitili maanani yoyote matendo ya mtu yeyote. Badala yake, Mimi hufanya kazi Ninayopaswa kufanya, iwe kukusanya habari, kuzunguka katika nchi au kufanya jambo ambalo linanipendeza. Katika nyakati muhimu, Mimi huendelea na kazi Yangu miongoni mwa wanadamu kama ilivyopangwa awali, bila kuchelewa au kuwa mapema hata kidogo, na kwa urahisi na kwa makini. Hata hivyo, katika kila hatua ya kazi Yangu, watu wengine wanawekwa pembeni, kwa sababu Ninadharau hali yao ya kujipendekeza na hali yao ya kujifanya wanyenyekevu. Wale wanaonichukiza sana hakika watatelekezwa, iwe ni kwa kupenda au kwa kutopenda. Kwa ufupi, Ningependa wale wote Ninaowadharau wawe mbali sana Nami. Ni dhahiri kwamba, Sitawahurumia wale waovu ambao wamebaki katika nyumba Yangu. Kwa kuwa siku ya adhabu ya mwanadamu inakaribia, Sina haraka ya kuzitupa nje zile nafsi zote zinazostahili dharau kutoka katika nyumba Yangu, kwa kuwa Nina mpango Wangu mwenyewe.

Huu ndio wakati Ninapoamua mwisho wa kila mtu, bali si hatua ambapo nilianza kumfanyanga mwanadamu. Mimi huandika maneno na matendo ya kila mtu katika kitabu Changu, moja baada ya lingine, njia ambayo kwayo wameitumia kunifuata, sifa zao asilia, na hatimaye jinsi ambavyo wamejistahi. Kwa njia hii, haijalishi ni mtu wa aina gani, hakuna mtu yeyote atakayeepuka mkono Wangu, na wote watakuwa pamoja na wa aina yake kama Nilivyopanga. Ninaamua hatima ya kila mtu si kwa kuzingatia umri, ukubwa, kiwango cha mateso, sembuse kiwango ambacho kwacho anataka huruma, bali kulingana na ikiwa anao ukweli. Hakuna chaguo lingine ila hili. Sharti mtambue kwamba wale wote ambao hawafuati mapenzi ya Mungu wataadhibiwa pia. Huu ni ukweli usiobadilika. Kwa hivyo, wale wote wanaoadhibiwa wanaadhibiwa kwa ajili ya haki ya Mungu na kama malipo kwa ajili ya vitendo vyao vingi viovu. Sijafanya mabadiliko yoyote katika mpango Wangu tangu uanzishwe. Ni

kwamba tu, kwa binadamu, wale ambao kwao Mimi huelekeza maneno Yangu wanaonekana kupungua kwa idadi, sawa na wale Ninaowakubali kwa kweli. Hata hivyo, Ninasisitiza kwamba mpango Wangu haujawahi kubadilika; badala yake, ni imani na upendo wa mwanadamu ambavyo hubadilika daima, kufifia daima, kiasi kwamba kuna uwezekano wa kila mwanadamu kubadilika kutoka kujipendekeza Kwangu hadi kufikia hali ya kunidharau au hata kunitupa nje. Mtazamo Wangu kwenu hautakuwa baridi wala moto, hadi pale Nitakapohisi kuchukizwa na karaha, na hatimaye kutoa adhabu. Hata hivyo, katika siku ya adhabu yenu, bado Nitawaona lakini nyinyi hamtaweza kuniona tena. Kwa kuwa maisha miongoni mwenu yameshakuwa ya kuchosha na ya taabu Kwangu, basi, ni wazi kwamba Nimechagua mazingira tofauti ya kuishi, afadhali kuepuka kuumizwa na maneno yenu maovu na kuwa mbali na tabia zenu mbovu kwa namna isiyovumilika, ili msinipumbaze au kunitendea kwa namna ya uzembe tena. Kabla Sijawaacha, lazima bado Ninawasihi mjiepushe kufanya yale ambayo hayaambatani na ukweli. Badala yake, mnafaa kufanya kile ambacho kinawapendeza wote, kile kilicho na manufaa kwa wote, na kile kinachofaidi hatima yenu wenyewe, la sivyo, yule anayeteseka katika maafa hatakuwa mwingine ila wewe.

Huruma Yangu inaonyeshwa kwa wale wanaonipenda Mimi na kujinyima. Kwa sasa, adhabu itakayowapata waovu, ni thibitisho hasa la tabia Yangu ya haki na, hata zaidi, ushuhuda wa hasira Yangu. Msiba utakapofika, wote wanaonipinga watalia watakapokumbwa na njaa na baa. Wale ambao wametenda aina zote za uovu, lakini ambao wamenifuata kwa miaka mingi, hawataepuka kulipia dhambi zao; wao pia, watatumbukia katika maafa, ambayo yameonekana kwa nadra kotekote katika mamilioni ya miaka, na wataishi katika hali ya taharuki na woga daima. Na wale kati ya wafuasi Wangu ambao wamekuwa waaminifu Kwangu watafurahi na kushangilia ukuu Wangu. Watakuwa na ridhaa isiyo na kifani na kuishi kwa raha ambayo Sijawahi kuwapa wanadamu. Kwa sababu Ninathamini matendo mema ya mwanadamu na kuchukia matendo yake maovu. Tangu Nilipoanza kuwaongoza wanadamu, Nimekuwa Nikitamani kwa hamu kupata kikundi cha watu ambao wanafikiria kama Mimi. Wale ambao hawana fikira sawa na Zangu, wakati ule ule, Siwasahau kamwe; Ninawachukia kabisa moyoni Mwangu daima, Nikisubiri nafasi ya kutoa adhabu kwao, jambo ambalo Nitafurahia kuona. Sasa siku Yangu imefika hatimaye, na Sihitaji kusubiri zaidi!

Kazi Yangu ya mwisho si kwa ajili ya kumwadhibu mwanadamu tu bali pia kwa ajili ya kupanga hatima ya mwanadamu. Aidha, ni kwa ajili ya kupokea shukrani kutoka kwa kila mtu kwa yale yote ambayo Nimefanya. Ninataka kila mtu aone kwamba yale yote ambayo Nimefanya ni sahihi na kwamba yote ambayo Nimefanya ni dhihirisho la tabia Yangu; si kwa uwezo wa mwanadamu, sembuse ulimwengu, ambao uliwaleta wanadamu. Kinyume na hili, mimi Ndiye Ninalisha kila kiumbe miongoni mwa vitu vyote. Bila uwepo Wangu, wanadamu

wataangamia tu na kusumbuka kutokana na mashambulizi ya misiba. Hamna mwanadamu atakayeona uzuri wa jua na mwezi au dunia ya kijani kibichi; wanadamu watakumbana tu na usiku wenye baridi na bonde kali la uvuli wa mauti. Mimi tu Ndiye wokovu wa wanadamu. Mimi tu ndiye tumaini la wanadamu na zaidi ya hayo; Mimi tu Ndiye mwamba wa uwepo wa wanadamu wote. Bila Mimi, wanadamu watasimama kabisa mara moja. Bila mimi, wanadamu watakumbana na msiba mkuu na kukanyagwa na mapepo wa aina yote, hata kama hamna anayenisikiliza. Nimefanya kazi ambayo haiwezi kufanywa na yeyote yule ila mimi. tumaini Langu la pekee ni kwamba mwanadamu anaweza kunilipa kwa kutenda matendo kiasi mema. Ingawa wanaoweza kunilipa ni wachache, bado Nitahitimisha safari Yangu duniani na Nianze hatua ifuatayo ya kazi Yangu inayotokea, kwa sababu kukimbia kimbia Kwangu miongoni mwa wanadamu kwa miaka hii mingi imekuwa na matokeo mazuri, na Nimefurahishwa sana. Sijali kuhusu idadi ya watu ila kuhusu matendo yao mazuri. Kwa hali yoyote ile, Ninatumaini kwamba mtatayarisha matendo mema ya kutosha kwa ajili ya hatima yenu wenyewe. Huo ndio wakati Nitakaporidhika; la sivyo, hakuna yeyote miongoni mwenu atakayepuka maafa yatakayowafikia. Maafa haya hutoka Kwangu na bila shaka Mimi ndiye Niliyeyapanga. Ikiwa hamwezi kuonekana kuwa wema mbele Yangu, basi hamtaweza kuyaepuka maafa. Wakati wa majonzi, vitendo vyenu havikuchukuliwa kama vinavyofaa kabisa, kwa sababu imani na upendo wenu vilikuwa tupu, na mlilionyesha tu kuwa wenye woga au sugu. Kuhusu hili, Nitafanya hukumu ya mazuri au mabaya tu. Shaka Yangu inaendelea kuwa jinsi kila mmoja wenu hutenda na kujionyesha, kwa msingi ambao Nitatumia kufanya uamuzi kuhusu hatima yenu. Hata hivyo, ni sharti Niseme wazi kwamba: Sitawahurumia tena wale ambao hawakuwa waaminifu Kwangu kabisa wakati wa majonzi, kwa sababu huruma Yangu ina mipaka. Zaidi ya hayo, Simpendi yeyote yule ambaye amewahi kunisaliti Mimi, wala Sipendi kujihusisha na wale ambao hawawajali wenzao. Bila kujali huyo mtu ni nani, hii ndiyo tabia Yangu. Ni lazima Niwaambie hili: Yeyote atakayehuzunisha moyo Wangu hatapokea huruma kutoka Kwangu mara ya pili, na yeyote ambaye amekuwa mwaminifu Kwangu atadumu moyoni Mwangu milele.

Wewe U Mwaminifu kwa Nani?

Kila siku mnayoiishi sasa ni ya maana sana na muhimu sana kwa hatima yenu na majaliwa yenu, kwa hivyo mnapaswa kufurahia kila mlichio nacho na kila dakika inayopita. Mnapaswa kutumia muda wenu vizuri ili muweze kujinufaisha, ili msije kuishi maisha haya bure. Pengine mnajihisi kukanganyikiwa mnaojiuliza ni kwa nini Ninazungumza maneno haya. Kwa kweli, Sijapendezwa na matendo ya yeyote kati yenu. Kwa maana matumaini ambayo Nimekuwa nayo juu yenu si vile tu mlivyo sasa. Kwa hivyo, Naweza kuelezea hivi: Nyinyi nyote mko hatarini kabisa. Vilio vyenu vya kwanza kwa ajili ya wokovu na matamania yako ya kwanza ya kufuatilia ukweli na kutafuta nuru vinakaribia mwisho. Hivi ndivyo mtakavyonifidia mwishowe,

ambacho ni kitu ambacho Sijawahi kutarajia. Sitamani kuzungumza kinyume cha ukweli, kwa maana mmenivunja moyo sana. Pengine hampendi kuiachia mada hapo na hutaki kuukabili ukweli, lakini ni lazima niwaulize swali hili: Kwa miaka hii yote, mioyo yenu imejawa na nini? Mioyo yenu inamwamini nani? Usiseme kwamba swali Langu limekuja ghafla sana, na usiniulize kwa nini Nauliza swali kama hilo. Mnapaswa kujua hili: Ni kwa sababu Ninawafahamu vizuri, ninawajali sana, na Ninajitolea moyo Wangu sana kwa kile mnachofanya, ndio maana Ninawauliza kwa kurudiarudia na kubeba taabu isiyoелеzeka. Hata hivyo, malipo Yangu yamekuwa ni kupuuzwa na kukataliwa kusikostahimilika. Hivyo mmekuwa na ajizi sana juu Yangu; Ninawezaje kutojua kitu kuhusu hilo? Kama mnaamini kwamba hili linawezekana, inathibitisha ukweli zaidi kwamba hamnitendei wema kabisa. Kisha Ninawaambia kwamba mnajidanganya nyinyi wenyewe. Nyinyi nyote ni werevu sana kiasi kwamba hamjui kile mnachofanya; sasa mtatumia nini ili kunipatia ufafanuzi?

Swali muhimu sana kwangu ni mioyo yenu inamwamini nani. Pia Ningependa kila mmoja wenu afikiri vizuri na kisha ajiulize uaminifu wake uko kwa nani na anaishi kwa ajili ya nani? Pengine hamjawahi kuliangalia swali hili kwa makini, hivyo nitawapatia jibu lake.

Wale wenye kumbukumbu nzuri wataukubali ukweli huu: Mwanadamu anaishi kwa ajili yake mwenyewe na ni mwaminifu kwake mwenyewe. Siamini kwamba jibu lenu ni sahihi kabisa, kwa maana kila mmoja wenu anaishi maisha yake, kila mmoja wenu anapambana katika dhiki yake. Kwa hivyo, kile mnachokuwa waaminifu kwacho ni watu mnaowapenda, na vitu vinavyowapendeza, na wala nyinyi si waaminifu kwa nafsi zenu wenyewe. Kwa sababu kila mmoja wenu anaathiriwa na watu, matukio, na vitu vinavyowazunguka, kimsingi nyinyi si waaminifu kwa nafsi zenu. Nasema maneno haya siyo kwa sababu ya kuunga mkono ninyi kuwa waaminifu kwa nafsi zenu, bali kufichua uaminifu wenu kwa kitu chochote kile. Maana kwa miaka yote hii Sijawahi kupokea uaminifu kutoka kwa mtu yeyote kati yenu. Mmekuwa wafuasi Wangu kwa miaka mingi sana, lakini hamjawahi kunionesha hata chembe ya uaminifu. Badala yake mmekuwa mkizunguka kwa watu mnaowapenda na vitu vinavyowapendeza sana, na kuviweka karibu na mioyo yenu na havijawahi kuachwa, wakati wowote, mahali popote. Mnapokuwa na hamu ama shauku na kitu chochote kile Mnachokipenda, siku zote mnakuwa ni wakati ambapo mnanifuata, au hata wakati mnaposikiliza maneno Yangu. Hivyo nasema, mnatumia uaminifu ninaowataka muonyeshe, kuwa badala yake waaminifu na kufurahia “vipenzi” wenu. Ingawa mnaweza kutoa sadaka ya kitu kimoja au vitu viwili kwa ajili Yangu, hakuwakilishi vitu vyenu vyote, na haionyeshi kwamba ni Kwangu ambako uaminifu wako uko kwa kweli. Mnajiweka wenyewe katika shughuli ambazo mnazipenda: Wengine ni waaminifu kwa watoto, wengine kwa waume, wake, utajiri, kazi, wenye vyeo, umaarufu, au wanawake. Kwa maana kile ambacho mnakuwa waaminifu kwacho, hujawahi kuhisi kuchoshwa au kukerwa

nacho, badala yake, mnatamani kuwa na kiasi kikubwa zaidi na ubora wa vitu ambavyo ninyi mu waaminifu kwavyo na hamjawahi kukata tamaa. Mimi mwenyewe na maneno Yangu daima hutupwa pembeni katika masuala ya vitu mnavyovipenda. Na hamna namna isipokuwa kuyaweka mwisho; wengi hata wanaondoka sehemu ya mwisho kwa ajili ya kuwa waaminifu kwa kitu ambacho hawajakigundua bado. Hawajawahi kuniweka mioyoni mwao kwa kiwango chochote kile. Pengine mtafikiri kwamba ninahitaji mambo mengi sana kutoka kwenu au Ninawahukumu kimakosa, lakini je, mmeshawahi kufikiri kuhusu ukweli huu kwamba mnapotumia muda kwa furaha pamoja na familia yenu, hujawahi kuwa mwaminifu kwangu hata mara moja? Wakati kama huu, hii haiwaumizi? Mioyo yenu inapojawa na furaha kwa kupokea malipo kwa kazi zenu, haiwavunji moyo kwamba hamjajitweka kwa ukweli wa kutosha? Ni lini mmewahi kulia kwa kukosa idhinisho langu? Mnaitesa akili yenu na kupata maumivu makubwa kwa ajili ya watoto wenu, lakini bado hamjaridhika, bado mnaamini kwamba hamjaweka jitihada za kutosha kwao, kwamba hamjatumia nguvu zenu zote. Lakini Kwangu, mmekuwa ajizi na wa kutojali, mkiniweka tu katika kumbukumbu zenu na wala Sidumu ndani ya mioyo yenu. Kujitolea Kwangu na jitihada zangu daima hupita bila nyinyi kuzihisi, na wala hamjawahi kuweka jitihada ili muweze kuelewa. Nyinyi hutafakari kidogo tu na kuamini kwamba hiyo itatosha. “Uaminifu” wa aina hii sio ule ambao Nimekuwa nikiutazamia, bali ni ule ambao umekuwa machukizo Kwangu kwa muda mrefu. Hata hivyo, licha ya kile Ninachokisema, mtaendelea kukubali kitu kimoja tu au vitu viwili na kushindwa kukikubali kwa ukamilifu, kwa maana nyote “mnajiamini” sana, na siku zote mnachagua kipi mtakachokikubali kutoka katika maneno Niliyoyasema. Kama bado mko hivi, Nina njia katika akiba za kukabiliana na kujiamini kwenu, na Nitazitumia ili muweze kuyatambua maneno Yangu yote kuwa ni kweli na sio upotoshaji wa ukweli.

Kama sasa Ningeweka utajiri mbele yenu na kuwaambia kuwa mchague kwa uhuru, huku Nikijua kwamba^[a] sitawahukumu, basi wengi wangechagua utajiri na kuacha ukweli. Wazuri miongoni mwenu wangeacha utajiri na kuchagua ukweli shingo upande, ilhali wale ambao wako katikati wangekumbatia utajiri kwa mkono mmoja na kwa mkono mwingine kuukumbatia ukweli. Kwa njia hii, je, rangi zenu halisi si zingejidhihirisha? Unapochagua ukweli kwa kulinganisha na kitu chochote ambacho u mwaminifu kwacho, wote mtafanya maamuzi kama hayo, na tabia yenu itabakia kuwa ile ile. Si ndivyo ilivyo? Je, hakuna watu wengi miongoni mwenu waliobadilika badilika katika kuchagua baina ya wema na ubaya? Katika mashindano kati ya mazuri na mabaya, nyeusi na nyeupe, mna uhakika na uchaguzi mlioufanya kati ya familia na Mungu, watoto na Mungu, amani na vurugu, utajiri na umasikini, hadhi na kuwa mtu wa kawaida, kusaidiwa na kutupiliwa mbali, na kadhalika. Kati ya familia yenye amani na familia iliyovunjika, nyinyi huchagua ya kwanza bila kusita; kati ya utajiri na wajibu, safari hii

pia mnachagua ya kwanza, bila kuwa na nia ya kurudi ufuoni^[b] kati ya starehe na umasikini, tena mlichagua ya kwanza; kati ya watoto, mke, mume na Mimi, mnachagua za kwanza; na kati ya dhana na ukweli, kwa mara nyingine tena mlichagua ya kwanza. Nikikabiliwa na kila namna ya matendo yenu maovu, karibu sana Nimepoteza imani Yangu kwenu. Ninashangazwa sana na kwamba mioyo yenu inapinga kulainishwa. Miaka mingi ya kujitolea na jitihada Yangu imeniletea kuvunjika moyo tu nanyi kupoteza imani Nami. Hata hivyo, matumaini Yangu juu yenu yanakua kila siku inayopita, kwa kuwa siku Yangu tayari imekwisha kuwekwa wazi kwa kila mtu. Lakini, bado mnaendelea kuyafuata yale ambayo ni ya giza na maovu, na mnakataa kulegeza mshiko wenu. Kwa kufanya hivyo, mtapata matokeo gani? Mmewahi kutafakari kwa makini kuhusu hili? Kama mngetakiwa kuchagua tena, msimamo wenu ungekuwa upi? Bado lingekuwa ni chaguo la kwanza? Je, yale ambayo mngenipatia bado yangekuwa maudhi na huzuni ya majuto? Je, mioyo yenu bado ingekuwa migumu? Je bado mngekuwa hamjui cha kufanya ili kuufariji moyo Wangu? Kwa wakati wa sasa, chaguo lenu ni nini? Mtayakubali maneno Yangu, au yatawachosha? Siku Yangu imewekwa wazi kabisa mbele ya macho yenu, na kile mnachokiona ni maisha mapya na mwanzo mpya. Hata hivyo, ni lazima niwaambie kwamba huu mwanzo mpya si mwanzo wa kazi mpya iliyopita, bali ni mwisho wa ya kale. Yaani, hili ni tendo la mwisho. Ninaamini nyote mtaelewa kitu ambacho si cha kawaida kuhusu mwanzo huu mpya. Lakini siku moja hivi karibuni, mtaelewa maana halisi ya huu mwanzo mpya, kwa hivyo hebu sote tuipite na kuikaribisha tamati inayofuata! Hata hivyo, kitu ambacho Ninaendelea kutofurahishwa nacho ni kwamba pale mnapokabiliwa na mambo ambayo si ya haki na mambo ya haki, daima mmekuwa mkichagua chaguo la kwanza. Lakini hayo yote yako katika maisha yenu ya zamani. Pia Ninatumai kuyasahau yale yote yaliyotokea katika maisha yenu ya zamani, kitu kimoja baada ya kingine, ingawa hili ni gumu sana kufanya. Lakini bado nina njia nzuri sana ya kulitimiza. Acha maisha ya baadaye yachukue nafasi ya maisha ya zamani na kuacha kivuli cha maisha yenu ya zamani kiondolewe badala ya utu wenu halisi wa leo. Hii ina maana kwamba nitawasumbua tena ili uweze kufanya maamuzi kwa mara nyingine tena na tutaona kabisa nyinyi ni waaminifu kwa nani.

Tanbihi:

a. Matini ya asili haina kauli “kuelewa kwamba.”

b. Kurudi ufuoni: nahau ya Kichina, ikiwa na maana kwamba “mtu kuacha njia zake za uovu.”

Juu ya Hatima

Wakati wowote hatima inatajwa, muichukulie kwa uzito maalumu; nyinyi nyote ni mahususi hasa kuhusu jambo hili. Baadhi ya watu hawawezi kusubiri kumsujudia Mungu ili hatimaye kuwa na hatima nzuri. Naweza kutambua hamu yenu, ambayo haihitaji kuonyeshwa

katika maneno. Kabisa hamtaki miili yenu ianguke katika maafa, na hata zaidi, hamtaki kushuka katika adhabu ya muda mrefu hapo baadaye. Mnatarajia tu kujiruhusu muishi kwa uhuru zaidi kidogo, kwa urahisi zaidi kidogo. Na hivyo unahisi mwenye wasiwasi hasa wakati wowote hatima inatajwa, ukiwa na hofu kubwa kwa undani kwamba, usipokuwa mwangalifu vya kutosha, unaweza kumkosea Mungu na hivyo upate adhabu unayostahili. Hamjasita kufanya maafikiano kwa ajili ya hatima zenu, na wengi wenu ambao wakati mmoja walikuwa wa kuzunguka na wapuuzi hata kwa ghafla wamegeuka hususa wapole na wa dhati; unyofu wenu hata una mzizimo. Pasipo kutilia maanani, nyinyi nyote mna mioyo “minyooofu”, na kutoka mwanzo hadi mwisho mmejifungua wazi Kwangu bila kuficha siri zozote katika mioyo yenu, yawe lawama, udanganyifu, au ibada. Kwa jumla, “mmekiri” kwa uwazi Kwangu yale mambo muhimu katika pahali pa siri yenye kina kwenu. Mambo kama yalivyo, Sijawahi kuepuka mambo kama haya, kwa sababu yamekuwa ya kawaida Kwangu. Afadhali muingie katika bahari la moto kwa hatima yenu ya mwisho kuliko kupoteza mlia mmoja wa nywele ili kupata kibali cha Mungu. Sio kwamba Ninakuwa wa kulazimishia imani kwenu; ni kwamba mioyo yenu ya ibada ni pungufu hasa kwa kukabiliana na kila kitu Ninachofanya. Hamuwezi kuelewa Ninachomaanisha, hivyo basi acheni Niwatolee maelezo rahisi: Mnachohitaji si ukweli na maisha; si kanuni za jinsi ya kutenda, na hasa siyo kazi Yangu yenye kujitahidi. Yote mnayohitaji ni yale ambayo mnamiliki katika mwili—mali, hadhi, familia, ndoa, nk. Ninyi mnatupilia mbali kabisa maneno na kazi Yangu, hivyo Naweza kujumlisha imani yako kwa neno moja: shingo upande. Mtafanya lolote ili kutimiza mambo ambayo bila shaka mmejitolea, lakini Nimegundua kwamba hampuuzi kila kitu kwa ajili ya mambo ya imani yenu katika Mungu. Badala yake, nyinyi ni waaminifu tu kiasi, na kiasi. Hiyo ndiyo sababu Nasema kwamba wale wanaokosa moyo wa usafi mkubwa ni washinde katika imani yao katika Mungu. Fikiria kwa uangalifu—je, kuna wengi washinde miongoni mwenu?

Mnapaswa kujua kwamba mafanikio katika kumwamini Mungu yanatimizwa kwa sababu ya matendo ya watu wenyewe; wakati watu hawafanikiwi lakini badala yake wanashindwa, hiyo pia ni kwa sababu ya matendo yao wenyewe, sio matokeo ya vipengele vingine. Ninaamini kwamba mngefanya kitu chochote kitachukua ili kupata kitu kufanyika ambacho ni kigumu zaidi na kinachohitaji mateso zaidi kuliko kumwamini Mungu, na kwamba mngekichukulia kwa makini sana. Hamngetaka hata kufanya makosa yoyote; hizi ni aina za juhudi zisizolegea ambazo nyote mmeweka katika maisha yenu wenyewe. Nyinyi hata mna uwezo wa kunidanganya Mimi katika mwili chini ya hali ambazo hamuwezi kudanganya yeyote wa familia yenu wenyewe. Hii ni tabia yenu thabiti na kanuni ambayo mnatumia katika maisha yenu. Je, si bado mnaendeleza picha ya uongo ili kunidanganya Mimi, kwa ajili ya hatima yenu, na kuwa na hatima nzuri na ya furaha? Nafahamu kwamba ibada yenu na unyofu wenu ni wa muda tu; je, matamania yenu na

gharama mnayolipa ni ya sasa tu na si ya baadaye? Mnataka tu kutumia nguvu moja ya mwisho ili kupata hatima nzuri. Azma yenu ni kubadilisha tu; siyo ili msiwe wenye deni kwa ukweli, na ni hasa msinilipe kwa ajili ya gharama Niliyolipa. Kwa neno, mko tu tayari kutumia ujanja wenu, lakini hamtaki kuipigania. Je, si haya ni matakwa yenu ya dhati? Sio lazima mjifiche, na hata zaidi, sio lazima mpige mbongo zenu juu ya hatima yenu hadi pale ambapo hamuwezi kula au kulala. Je, si ni kweli kwamba matokeo yenu yatakuwa yameamuliwa mwishowe? Mnapaswa kufanya wajibu wenu wenyewe kwa kadri ya uwezo wenu kwa mioyo iliyo wazi na wima, na muwe tayari kufanya chochote kitakachohitajika. Kama mlivyosema, wakati siku itakuja, Mungu hatakosa kumjali mtu yeyote ambaye aliteseka au kulipa gharama kwa ajili Yake. Aina hii ya imani ni yenye thamani kuishikilia, na hampaswi kuisahau kamwe. Ni tu kwa njia hii Ninaweza kutuliza akili Yangu kuwahusu. Vinginevyo, Sitakuwa na uwezo wa kutuliza akili Yangu kuwahusu, na milele mtakuwa malengo ya chuki Yangu. Kama nyote mnaweza kufuata dhamiri zenu na kutoa yote kwa ajili Yangu, msiwache jitihada zozote kwa ajili ya kazi Yangu, na kutenga maisha ya jitihada za kazi ya injili Yangu, basi si moyo Wangu mara kwa mara utaruka kwa furaha kwa ajili yenu? Si Mimi Nitakuwa na uwezo wa kutuliza akili Yangu kuwahusu? Ni aibu kwamba kile mnaweza kufanya ni cha kusikitisha sana na sehemu ndogo sana ya kile Ninachotarajia; hivi sasa, ni jinsi gani mna nyongo ya kutafuta kutoka Kwangu kile mnatumainia?

Hatima yenu na majaliwa yenu ni muhimu sana kwenu—ni za matatizo makubwa. Mnaamini kuwa msipofanya mambo kwa uangalifu sana, itakuwa sawa na kutokuwa na hatima, na uharibifu wa majaliwa yenu. Lakini mmewahi kufikiri kwamba kama juhudi mtu hutumia ni kwa ajili ya hatima zao tu, hizo ni kazi tu zisizo na matunda? Juhudi za aina hiyo si halisi—ni bandia na danganyifu. Kama ni hivyo, wale ambao wanafanya kazi kwa ajili ya hatima yao watapokea maangamizo yao ya mwisho, kwa sababu kushindwa katika imani ya watu katika Mungu hutendeka kwa sababu ya udanganyifu. Hapo awali Nilisema kuwa Mimi Sipendi kusifiwa mno au kupendekezwa, au kuchukuliwa kwa shauku. Ninapenda watu waaminifu kukubali hali ilivyo kuhusu ukweli na matarajio Yangu. Hata zaidi, Ninapenda wakati watu wanaweza kuonyesha uangalifu mkubwa na kufikiria kwa ajili ya moyo Wangu, na wakati wanaweza hata salimisha kila kitu kwa ajili Yangu. Ni kwa njia hii tu ndipo Moyo wangu unaweza kuliwazwa. Sasa hivi, ni mambo mangapi yapo yanayowahusu ambayo Mimi Nachukia? Ni mambo mangapi yapo yanayowahusu ambayo Napenda? Je, hakuna kati yenu ambaye ametambua ubaya wote ambao mmeonyesha kwa ajili ya hatima zenu?

Katika moyo Wangu, Sitaki kuwa Mwenye kudhuru moyo wowote ambao ni chanya na wa motisha, na Mimi hasa Sitaki kupunguza bidii ya mtu yeyote ambaye anafanya wajibu wake kwa uaminifu; hata hivyo, ni lazima Niwakumbushe kila mmoja wenu juu ya upungufu wenu na roho

chafu sana ndani ya mioyo yenu. Azma ya kufanya hivyo ni kutarajia kwamba mtaweza kutoa mioyo yenu ya kweli katika kukabiliana na maneno Yangu, kwa sababu kile Nachukia zaidi ni udanganyifu wa watu kuelekezwa Kwangu. Natarajia tu kuwa katika hatua ya mwisho ya kazi Yangu, mnaweza kutekeleza kwa kujitokeza, kujitoa kikamilifu, na wala sio shingo upande tena. Bila shaka, Natarajia pia kuwa nyote muwe na hatima nzuri. Hata hivyo, bado Nina mahitaji Yangu ambayo ni kwenu nyinyi mfanye uamuzi bora kabisa katika kujitoa Kwangu pekee na moyo wa ibada ya mwisho. Kama mtu hana moyo huo wa ibada pekee, mtu huyo hakika atakwenda kuwa thamani ya Shetani, na Mimi Sitaendelea kumtumia. Nitamtuma nyumbani akatunzwe na wazazi wake. Kazi yangu imekuwa ya msaada sana kwa ajili yenu; kile Natarajia kupata kutoka kwenu ni moyo ulio mwaminifu na unaotia msukumo kwenda juu, lakini hadi sasa mikono Yangu bado ni tupu. Fikiria kulihusu: Wakati siku moja bado Nitakuwa na kukwazika kusikoelezeka, mtazamo Wangu kuwaelekea utakuwa upi? Je, Mimi bado Nitakuwa mwema? Je, Moyo wangu utakuwa bado mtulivu? Je, mnaelewa hisia za mtu ambaye kwa kujitahidi amelima lakini hakuvuna hata nafaka moja? Je, mnaelewa ukubwa wa jeraha la mtu ambaye amepigwa kipigo kikubwa? Je, mnaweza kuonja uchungu wa mtu aliyejawa na matumaini ambaye anafaa kuachana na mtu kwa uhusiano mbaya? Je, mmeona hasira ya mtu ambaye amekasirishwa? Je, mnaweza kujua hisia ya kulipiza kisasi kwa haraka ya mtu ambaye amekuwa akichukuliwa kwa uadui na udanganyifu? Kama mnaelewa fikira za watu hawa, Nadhani haipaswi kuwa vigumu kwenu kuwaza mtazamo Mungu Atakuwa nao wakati ule wa adhabu Yake. Hatimaye, Natarajia nyote mnaweka jitihada kali kwa ajili ya hatima yenu wenyewe; hata hivyo, ni bora msitumie njia za udanganyifu katika juhudi zenu, au bado Nitasikitishwa nanyi katika moyo Wangu. Je, kusikitishwa kwa aina hii huelekea wapi? Je, hamjidanganyi wenyewe? Wale ambao hufikiria kuhusu hatima yao na bado wanaiharibu ni watu wenye uwezekano mdogo zaidi wa kuokolewa. Hata kama watu hawa watakerwa, ni nani atawahurumia? Kwa jumla, bado Niko tayari Kuwatakia muwe na hatima inayofaa na nzuri. Hata zaidi, Natarajia kwamba hakuna kati yenu atakayeanguka katika maafa.

Maonyo Matatu

Kama muumini wa Mungu, hufai kuwa watiifu kwa yeyote mwingine isipokuwa Yeye katika mambo yote na mjilinganishe na moyo Wake katika mambo yote. Hata hivyo, ingawa wote huelewa mafundisho haya, ukweli huu wa kimsingi ulio wazi kabisa kwa binadamu hauwezi kuonekana kuwa kujumuishwa kwao kikamilifu, kutokana na ugumu wao, kama vile hali yao ya kutojua, upuzi, au ufisadi. Kwa hivyo, kabla ya kuuamua mwisho wenu, Ninafaa kuwaambia kwanza baadhi ya mambo, ambayo ni yenye umuhimu mkubwa sana kwenu. Kabla Sijaendelea, mnafaa kwanza kuelewa yafuatayo: Maneno Ninayoongea ni ukweli unaoelekezwa kwa wanadamu wote, na wala hayajaelekezwa kwa mtu mahususi au aina fulani ya mtu. Kwa

hiyo, mnapaswa kumakinikia kupokea maneno Yangu kutoka katika mtazamo wa ukweli, na vile vile mdumishe mtazamo wa uzingativu na uaminifu kamili. Msipuuze hata neno moja au ukweli Ninaoongea, na wala usichukulie maneno Yangu kwa dharau. Katika maisha yenu, Naona mengi ambayo mnaifanya ambayo hayana uhusiano na ukweli, kwa hivyo Nawaambia moja kwa moja muwe watumishi wa ukweli na wala si kutawaliwa na maovu na ubaya. Msikanyage ukweli na kuchafua sehemu yoyote ya nyumba ya Mungu. Hili ndilo onyo Langu kwenu. Sasa Nitaanza kuzungumza kuhusu mada ya sasa:

Kwanza, kwa minajili ya majaliwa yenu, mnastahili kutafuta kuidhinishwa na Mungu. Hii ni kusema kwamba, kwa sababu mnatambua kwamba nyinyi mmehesabiwa miongoni mwa wale walio katika nyumba ya Mungu, basi mnastahili kumletea Mungu utulivu wa akili katika mambo yote na kumtosheleza katika kila jambo. Kwa maneno mengine, lazima muwe wenye maadili katika matendo yenu na kutii ukweli katika mambo kama hayo. Kama hali hii inazidi uwezo wako, basi utachukiwa na kukataliwa na Mungu na vilevile kukataliwa kwa dharau na kila mwanadamu. Punde utakapokuwa katika hali mbaya kama hii, basi hauwezi kuhesabiwa miongoni mwa wale walio kwenye nyumba ya Mungu. Hii ndiyo maana ya kutoidhinishwa na Mungu.

Pili, mnastahili kujua kwamba Mungu hupenda binadamu mwaminifu. Mungu ana kiini cha uaminifu, na kwa hivyo neno Lake siku zote linaweza kuaminika. Aidha, matendo Yake hayana dosari wala hayajadiliwi. Hii ndiyo maana Mungu anawapenda wale walio waaminifu kabisa Kwake. Uaminifu unamaanisha kumpa Mungu moyo wako; kutomdanganya katu katika kitu chochote; kuwa wazi Kwake katika mambo yote, kutowahi kuficha ukweli; kutowahi kufanya kile kinachowadanganya wale walio juu na kuwafumba macho wale walio chini; na kutowahi kufanya kile ambacho kinakupendekeza kwa Mungu. Kwa ufupi, kuwa waaminifu ni kujizuia dhidi ya uchafu katika matendo na maneno yenu, na kutomdanganya Mungu wala binadamu. Kile Ninachoongea ni rahisi sana lakini ni kigumu maradufu kwenu. Wengi wanaona afadhali washutumiwe hadi kuzimu kuliko kuongea na kutenda kwa uaminifu. Si ajabu kwamba Nina matendo mengine kwa wale ambao si waaminifu. Bila shaka, Ninaelewa ugumu mkuu mnaokumbana nao kwa kuwa binadamu waaminifu. Nyinyi wote ni werevu sana na stadi katika kupima uungwana wa mtu kwa kipimio chenu wenyewe; kwa hiyo kazi Yangu inakuwa rahisi zaidi. Na kwa sababu nyinyi mnaificha siri katika mioyo yenu, basi, Nitawatumeni, mmoja baada ya mwingine, katika janga kupitia ili “mfundishwe” kupitia moto, ili baadaye mtajitolea kabisa katika kuamini maneno Yangu. Hatimaye, Nitapokonya maneno “Mungu ni Mungu wa uaminifu,” kutoka kwa vinywa vyenu na kisha ndipo mtakapojigamba na kujitana kifua na kulalama, “Ujanja ndio moyo wa binadamu!” Hali za akili zenu zitakuwa zipi wakati huu? Ninafikiri hamtajisahau sana na majivuno kama mlivyo sasa. Na sembuse hamtakuwa “wa

maana sana kiasi cha kutoeleweka” kama mlivyo sasa. Baadhi hutenda kwa ustaarabu na huonekana hasa “wenye tabia nzuri” mbele ya Mungu, na bado wanakuwa waasi na wasiozuiliwa mbele ya Roho Mtakatifu. Je, mnaweza kumhesabu binadamu kama huyu miongoni mwa safu ya waaminifu? Kama wewe ni mnafiki na mmoja ambaye ni stadi katika kutangamana, basi Nasema kwamba bila shaka wewe ni mmoja ambaye humchezea Mungu. Kama maneno yako yamejaa visingizio na udhibitisho usio na thamani, basi Nasema kwamba wewe ndiwe ambaye huko radhi kabisa kuweka ukweli katika matendo. Kama wewe una siri nyingi usizotaka kutoa, na kama huko radhi kabisa kuweka wazi siri zako—yaani, ugumu wako—kwa wengine ili uweze kutafuta njia ya mwangaza, basi Ninasema kwamba wewe ni mmoja ambaye hatapokea wokovu kwa urahisi na ambaye hataweza kuibuka kutoka gizani kwa urahisi. Kama kutafuta njia ya ukweli kunakufurahisha vyema, basi wewe ni yule anayeishi kila mara katika mwangaza. Kama wewe unafurahia kuwa mtoa huduma katika nyumba ya Mungu, ukifanya kazi kwa bidii na kwa makini bila kuonekana, siku zote ukitoa na katu hupokei, basi Nasema kwamba wewe ni mtakatifu mwaminifu, kwani hutafuti tuzo na unakuwa tu binadamu mwaminifu. Kama uko radhi kuwa wazi, kama uko radhi kutoa kila kitu ulichonacho, kama una uwezo wa kujitolea maisha yako kwa ajili ya Mungu na kuwa shahidi, kama wewe ni mwaminifu hadi kwa kiwango ambapo unajua tu kumridhisha Mungu na si kujifikiria au kuchukua chochote kwa ajili yako, basi Nasema kwamba watu kama hao ndio wanaostawishwa na mwangaza na wataishi milele katika ufalme. Unafaa kujua kama kunayo imani ya kweli na uaminifu wa kweli ndani yako, kama una rekodi ya kuteseka kwa ajili ya Mungu, na kama umemtii Mungu kikamilifu. Kama unakosa hivi Nilivyotaja, basi ndani yako kunabaki kutotii, udanganyifu, ulafi, na kutotosheka. Kwa vile moyo wako si mwaminifu, hujawahi kupokea utambuzi mzuri kutoka kwa Mungu na hujawahi kuishi katika mwangaza. Kile ambacho jaala ya mtu kitakuwa hutegemea kama anao moyo wa uaminifu na wa kweli, na kama anayo nafsi isiyo na doa. Kama wewe ni mtu asiye mwaminifu sana, mtu mwenye moyo wa kijicho na nafsi isiyo safi, basi rekodi ya majaliwa yako bila shaka ipo pale ambapo binadamu huadhibiwa, jinsi ilivyoandikwa katika rekodi ya majaliwa yako. Kama unadai kwamba wewe ni mwaminifu sana, na bado kamwe hutendi kulingana na ukweli au kuongea neno la ukweli, basi bado unatarajia Mungu kukutuzi? Bado unatumai Mungu akuchukue kama kipenzi Chake? Je, kufikiria huku si kwa upuzi? Unamdanganya Mungu katika mambo yote, hivyo nyumba ya Bwana inawezaje kumpa nafasi mtu kama wewe, ambaye mikono yake si safi?

Jambo la tatu Ninalotaka kuwaambia ni hili: Kila mwanadamu, katika kuishi maisha yake ya imani katika Mungu, amemkataa na kumdanganya Mungu wakati fulani. Baadhi ya matendo mabaya hayahitaji kurekodiwa kama kosa, lakini mengine hayasameheki; kwani mengi ni yale yanayokiuka amri za utawala, yaani, yanaikosea tabia ya Mungu. Wengi ambao wanajali

majaliwa yao binafsi wanaweza kuuliza matendo haya ni yapi. Lazima mjue kwamba nyinyi mna kiburi na wenye majivuno kiasili, na hamko radhi kutii ukweli. Kwa sababu hii, Nitawaambia kidogo kidogo baada ya nyinyi kutafakari kujihusu. Ninawashawishi kuwa na ufahamu bora zaidi wa yaliyomo katika amri za utawala na kujua tabia ya Mungu. Vinginevyo, mtapata ugumu sana kuendelea kufunga vinywa vyenu na kufyata ndimi zenu dhidi ya kuropokwa bila kizuizi kwa mazungumzo ya mbwembwe, na bila kujua mtaikosea tabia ya Mungu na kujipata kwenye giza, mkipoteza uwepo wa Roho Mtakatifu na mwangaza. Kwa sababu nyinyi hamna maadili katika matendo yenu, kufanya na kutenda kile ambacho hufai kufanya hivyo, basi utapokea adhabu inayokufaa. Lazima ujue kwamba ingawa wewe ni mpotovu katika maneno yako na matendo yako, Mungu ni mwenye maadili sana katika hali hizi zote. Sababu ya wewe kupokea adhabu ni kwa sababu umemkosea Mungu na wala si binadamu. Kama, katika maisha yako, wewe hutenda makosa mengi dhidi ya tabia ya Mungu, basi huna budi ila kuwa mtoto wa kuzimu. Kwa binadamu inaweza kuonekana kwamba umetenda matendo machache tu yasiyolingana na ukweli na si chochote zaidi. Je, una habari, hata hivyo, kwamba katika macho ya Mungu, tayari wewe ni mmoja ambaye kwake hakuna tena sadaka ya dhambi? Kwani umevunja amri za utawala za Mungu zaidi ya mara moja na hujaonyesha ishara yoyote ya kutubu, kwa hivyo huna chaguo lolote ila kutumbukia kuzimu pale ambapo Mungu anamwadhibu mwanadamu. Katika wakati wao wa kufuata Mungu, idadi ndogo ya watu ilitenda matendo yaliyoenda kinyume na kanuni, lakini baada ya kushughulikiwa na kuongozwa, waligundua polepole upotovu wao, na kisha wakachukua njia iliyo sawa ya uhalisi, na leo wanabaki wenye msingi imara katika njia ya Bwana. Binadamu kama hawa ndio watakaobakia mwisho. Ni wale walio waaminifu ndio Ninaowatafuta; kama wewe ni mtu mwaminifu na unayetenda kwa maadili, basi unaweza kuwa msiri wa Mungu. Kama katika matendo yako huikosei tabia ya Mungu, na unatafuta mapenzi ya Mungu na unao moyo wa kumcha Mungu, basi imani yako ni ya kiwango kilichowekwa. Yeyote asiyemcha Mungu na asiye na moyo unaotetema kwa woga atakiuka amri za utawala za Mungu kwa urahisi. Wengi humhudumia Mungu kwa misingi ya hisia kali, na hawajui katu amri za utawala za Mungu, sembuse kuelewa athari za neno Lake. Na kwa hivyo, na nia zao nzuri, mara nyingi wanaishia kufanya vitu vinavyokatiza usimamizi wa Mungu. Kwa hali za uzito sana, wanatupwa nje na kunyang'anywa fursa yoyote zaidi ya kumfuata, na wanatupwa kuzimu bila ya kuwa na uhusiano wowote mwingine na nyumba ya Mungu unakoma. Watu hawa hufanya kazi katika nyumba ya Mungu wakiwa na nia nzuri zisizojua na wanaishia kuikasirisha tabia ya Mungu. Watu huleta njia zao za kuwahudumia wakuu na mabwana katika nyumba ya Mungu na kujaribu kufanya yatumike, wakidhania kwa kiburi kwamba njia kama hizo zinaweza kutumika hapa bila jitihada. Hawakuwahi kufikiria kwamba Mungu hana ile tabia ya mwanakondoo bali ile ya simba. Kwa hiyo, wanaojihusisha na Mungu kwa mara ya kwanza wanashindwa kuwasiliana na Yeye, kwani

moyo wa Mungu ni tofauti na ule wa binadamu. Ni baada tu ya kuelewa ukweli mwingi ndipo unapoweza kujua siku zote kumhusu Mungu. Maarifa haya si mafungu wala mafundisho, lakini yanaweza kutumika kama hazina ya kuingia katika matumaini ya karibu na Mungu, na ithibati kwamba Anafurahishwa na wewe. Kama unakosa uhalisi wa maarifa na hujajiandaa ukweli, basi huduma yako ya shauku itakuletea tu hali ya chuki ya kupindukia na kuchukizwa sana kwa Mungu. Sasa unafaa kuelewa kwamba imani katika Mungu si masomo tu ya teolojia.

Ingawa maneno Ninayotumia kuwaonya ni mafupi, vyote Nilivyovifafanua hapa ndivyo vinavyokosekana zaidi ndani yenu. Lazima mjue kwamba kile Ninachozungumzia sasa ni kwa minajili ya kazi Yangu ya mwisho miongoni mwa binadamu, kwa ajili ya kuamua hatima ya binadamu. Sipendelei kufanya kazi nyingi zaidi isiyo na maana, na wala Sipendelei kuendelea kuwaongoza wale binadamu wasio na matumaini kama mti uliooza, sembuse wale walio na nia mbaya kisiri. Pengine siku moja mtaelewa nia za dhati zinazoyasukuma maneno Yangu na michango ambayo Nimemfanyia mwanadamu. Pengine siku moja mtafahamu kanuni inayowawezesha kuamua hatima yenu binafsi.

Dhambi Zitamwelekeza Mwanadamu Jahanamu

Nimewapa maonyo mengi na kuwapa ukweli mwingi ili kuwashinda. Leo mnajihisi kustawishwa zaidi kuliko mlivyohisi hapo zamani, kuelewa kanuni nyingi za jinsi mtu anavyopaswa kuwa, na kumiliki kiasi kikubwa cha maarifa ya kawaida ambayo watu waaminifu wanapaswa kuwa nayo. Hiki ndicho mmepeka kwa miaka mingi sasa. Mimi sikani mafanikio yenu, lakini lazima Niseme wazi kuwa Mimi pia sikani kutotii na uasi wenu mwingi dhidi Yangu kwa hii miaka mingi, kwa sababu hakuna mtakatifu hata mmoja kati yenu, nyinyi pia ni watu mliopotoshwa na Shetani, na maadui wa Kristo. Dhambi zenu na kutotii kwenu hadi sasa havihesabiki, hivyo si ajabu kwamba daima Mimi hujirudia mbele yenu. Sitaki kuishi kuishi pamoja na nyinyi kwa namna hii—lakini kwa ajili ya siku zenu za baadaye, kwa ajili ya hatima zenu, hapa Nitarudia Niliyoyasema mara nyingine. Natumai mtaniendekeza, nami Natumai hata zaidi kwamba mtaweza kuamini kila neno Ninalosema, na bado zaidi, kwamba mtaweza kufahamu kwa kina maana ya maneno Yangu. Msiwe na shaka juu ya yale Ninayosema, au hata kuchukua maneno Yangu mnavyotaka na kuyatupilia mbali kwa hiari, jambo ambalo mimi Ninaona halistahimiliki. Msyahukumu maneno Yangu, wala kutoyachukulia kwa uzito, au kusema kwamba daima Nawajaribu, au mbaya zaidi, kusema kwamba kile ambacho Nimewaambia kinakosa usahihi. Ninaona kuwa mambo haya hayavumiliki. Kwa sababu mnanichukulia Mimi na kuyachukulia Ninayoyasema kwa shaka kuu na kamwe hamyazingatii, Ninamwambia kila mmoja wenu kwa uzito kabisa: Msiunganishe kile Ninachosema kwa falsafa, msikiweke pamoja na uongo wa matapeli, na hata zaidi, msijajibu maneno Yangu kwa dharau.

Labda katika siku zijazo hakuna mtu yeyote atakuwa na uwezo wa kuwaambia yale Ninayowaambia nyinyi, au kuzungumza na nyinyi kwa huruma sana, sembuse kuwaeleza mambo haya kwa uvumilivu hivi. Siku zijazo zitatumika katika kukumbuka nyakati zile nzuri, au kwa kulia kwa sauti kubwa, au kugumia kwa maumivu, au mtakuwa mkiishi katika usiku wa giza bila hata chembe ya ukweli au kupewa maisha, au kusubiri tu bila matumaini, au katika majuto machungu mengi kiasi kwamba hamwezi kufikiri.... Huu uwezekano mbadala hauwezi kuepukika kabisa kwa mtu yeyote kati yenu. Kwa sababu hakuna hata mmoja wenu ambaye anamiliki kiti ambacho kwacho kwa kweli mnamwabudu Mungu; mnajitumbukiza katika dunia ya uasherati na maovu, kuchanganya ndani ya imani yenu, ndani ya roho zenu, nafsi, na miili, mambo mengi yasiyohusiana na maisha na ukweli na kwa kweli yanapingana nayo. Hivyo kile Ninachotumai kwenu ni kuwa muweze kuletwa kwa njia ya mwanga. Tumaini Langu la pekee ni kwamba muweze kujitunza, muweze kujiangalia, si kuweka mkazo mwingi sana juu ya hatima yenu kiasi kwamba muitazame mienendo na dhambi zenu kwa kutojali.

Watu ambao wanamwamini Mungu kwa muda mrefu sasa wametumainia hatima iliyo nzuri, watu wote ambao wanamwamini Mungu wanatumai kwamba bahati nzuri itawajia ghafla, na wote wanatumai kwamba bila kujua, watajikuta wameketi kwa amani pahali pamoja au pengine mbinguni. Lakini Ninasema watu hawa kwa mawazo yao mazuri hawajawahi kujua kama wana sifa ya kupokea bahati nzuri kama hiyo inayoanguka kutoka mbinguni, au kukaa juu ya kiti huko mbinguni. Kwa sasa nyinyi mna maarifa mazuri kujihusu, lakini bado mnatarajia kwamba mnaweza kuepuka maafa ya siku za mwisho na mkono wa mwenye Uweza ukiwaadhibu wale waovu. Inaonekana kana kwamba kuwa na ndoto tamu na kutaka vitu kama tu wanavyopenda ni jambo la kawaida la watu wote ambao Shetani amewapotosha, si kipaji cha ajabu cha mtu fulani binafsi. Hata hivyo, bado Nataka kukomesha tamaa zenu badhirifu na hamu zenu za kupata baraka. Kwa kuwa dhambi zenu ni nyingi na ukweli wa kutotii kwenu ni mwingi na unaongezeka kila wakati, haya yanawezaje kupatana na ramani zenu nzuri za baadaye? Kama unataka kuendelea unavyopenda kuwa mwenye makosa, bila chochote kinachokuzuia, lakini bado unataka ndoto zitimie, basi Nakusihi uendelee katika usingizi wako na usiamke kamwe, kwa sababu unaota ndoto isiyoweza kutimia, na haitatumika kukufanya uwe mtu usiye wa kawaida mbele ya Mungu mwenye haki. Kama unataka tu ndoto zitimie, basi usiote kamwe, lakini kabiliana na ukweli milele, kabiliana na mambo ya hakika. Hiyo ndiyo njia ya pekee ya kukuokoa. Je, kwa maneno thabiti, hatua za taratibu hizi ni zipi?

Kwanza, fanya uchunguzi wa dhambi zako zote, na kuchunguza mwenendo na mawazo yako yote ambayo hayafuati ukweli.

Hiki ni kipengee ambacho mnaweza kukifanya kwa urahisi, na Ninaamini kwamba watu

wanaofikiri wanaweza kufanya hivi. Hata hivyo, wale watu ambao hawajui kamwe ni nini maana ya dhambi na ukweli ni tofauti, kwa sababu kimsingi wao si watu wa kufikiri. Mimi nazungumza na watu ambao wamethibitishwa na Mungu, ni waaminifu, hawajazikosea vibaya amri za utawala, na wanaweza kupata dhambi zao wenyewe kwa urahisi. Ingawa hiki ni kipengee ambacho Ninahitaji kwenu ambacho ni rahisi kwenu, sicho kipengee cha pekee Ninachohitaji kwenu. Lolote litokealo, Ninatumai kwamba hamtalicheka hitaji hili kwa siri, au hata zaidi, kwamba hamtaliangalia kwa dharau au kulichukulia kimzaha. Lichukulieni kwa umakini, na msilipuuze.

Pili, kwa kila moja ya dhambi na kutotii kwako tafuta ukweli unaoambatana na utumie ukweli huu kuzitatua, kisha badilisha vitendo vyako vya dhambi na mawazo yako na vitendo vya kutotii na kutenda ukweli.

Tatu, kuwa mtu mwaminifu, si mtu ambaye siku zote anakuwa mjanja, mwenye hila daima. (Hapa Ninakusihi tena uwe mtu mwaminifu.)

Kama unaweza kutimiza vipengee hivi vyote vitatu basi una bahati, wewe ni mtu ambaye ndoto zake zinatimia na ambaye hupata bahati nzuri. Labda mtayachukulia maombi haya matatu yasiyovutia kwa umakini, au labda mtayachukulia bila kuwajibika. Kwa vyovyote vile, azma Yangu ni kutimiza ndoto zenu, kuweka mawazo yenu katika matendo, si kuwadhihaki au kuwadanganya.

Madai Yangu yanaweza kuwa rahisi, lakini kile Ninachowaambia si rahisi hivyo kama kujumlisha moja na moja upate mbili. Kama mnazungumzia tu mambo haya bila kufikiria, mkiongea sana kwa kuparaganya kwa maneno matupu ya majivuno yanayopita kiasi, basi ramani zenu na matakwa yenu yatakuwa ukurasa mtupu milele. Mimi Sitakuwa na hisia ya huruma kwa wale kati yenu ambao wanateseka kwa miaka mingi na kufanya kazi kwa bidii bila matokeo yoyote. Kinyume cha hayo, Mimi Huwatendea wale ambao hawajatosheleza madai Yangu kwa adhabu, siyo zawadi, sembuse huruma yoyote. Labda mnawaza kwamba kwa kuwa wafuasi kwa miaka mingi mnaweka bidii bila kujali hali yoyote, hivyo kwa namna yoyote mnaweza kupata bakuli la wali katika nyumba ya Mungu kwa kuwa watendaji huduma. Ningesema wengi wenu mnafikiri hivi kwa sababu siku zote hadi sasa mmekuwa mkifuatilia kanuni ya jinsi ya kujinufaisha na jambo fulani na kutokuwa na manufaa kwa wengine. Hivyo Mimi nawaambia sasa kwa uzito kabisa: Sijali jinsi kazi yako ya bidii ni ya kusifiwa, jinsi sifa zako ni za kuvutia, jinsi unavyonifuata Mimi kwa karibu, jinsi ulivyo mashuhuri, au jinsi umeendeleza mwelekeo wako; mradi hujafanya kile ambacho Nimedai, hutaweza kupata sifa Zangu kamwe. Yafuteni hayo mawazo na hesabu zenu zote mapema iwezekanavyo, na muanze kuyachukulia madai Yangu kwa makini. Vinginevyo, Nitawafanya watu wote wawe majivu ili Niitamatishe kazi

Yangu, na hali ikiwa bora zaidi Niigeuze miaka Yangu ya kazi na kuteseka kuwa utupu, kwa sababu Siwezi kuwaleta katika ufalme Wangu maadui Wangu na watu waliojawa na maovu kwa mfano wa Shetani, katika enzi ijayo.

Nina matamania mengi. Natamani muweze kutenda kwa njia inayofaa na yenye mwenendo mzuri, muwe waaminifu kutimiza wajibu wenu, muwe na ukweli na ubinadamu, muwe watu ambao wanaweza kuacha vitu vyote na kuyatoa maisha yao kwa ajili ya Mungu, na mengineyo. Matumaini haya yote yanatokana na upungufu wenu na upotovu na kutotii kwenu. Kama kila mojawapo ya mazungumzo ambayo Nimekuwa nayo na nyinyi hayajatosha kuvuta nadhari yenu, basi huenda Sitasema mengine. Hata hivyo, nyinyi mnaelewa matokeo ya hayo. Sipumziki kamwe, kwa hiyo Nisiponena, Nitafanya kitu ili watu wakitazame. Ningeweza kuufanya ulimi wa mtu uoze, au mtu afe na viungo vyake kutolewa, au kumpa mtu kasoro za neva na kumfanya atende kama mwendawazimu. Au, basi tena, Ningeweza kufanya baadhi ya watu wavumilie maumivu makali Ninayowasababishia. Kwa njia hii Ningejihisi mwenye furaha, mwenye furaha sana na kufurahishwa sana. Imesemwa daima kwamba “Mema hulipizwa kwa mema, na maovu kwa maovu,” mbona isiwe hivyo sasa? Kama unataka kunipinga Mimi na unataka kutoa hukumu fulani kunihusu, basi Nitauozesha mdomo wako, na hilo litanipendeza Mimi sana. Hii ni kwa sababu mwishowe hujafanya lolote linalohusiana na ukweli, sembuse na maisha, ilhali kila kitu Ninachofanya ni ukweli, kila kitu kinahusiana na kanuni za kazi Yangu na amri za utawala Ninazoeleza rasmi. Kwa hiyo, Namsihi sana kila mmoja wenu kujilimbikiza wema kiasi, acha kufanya maovu mengi sana, na usikize madai Yangu katika wasaa wako. Kisha mimi Nitahisi furaha. Kama mngetoa (au kusaidia) kwa ukweli moja kwa elfu ya juhudi mnazoweka katika mwili, basi Nasema hungekuwa na dhambi mara kwa mara na midomo mbovu. Je, hili si dhahiri?

Kadri dhambi zako zilivyo nyingi, ndivyo nafasi zako za kupata hatima iliyo nzuri zilivyo chache. Kinyume chake, kadri dhambi zako zilivyo chache, ndivyo nafasi zako za kusifiwa na Mungu zilivyo nyingi. Kama dhambi zako zitaongezeka hadi kiwango ambapo haiwezekani Mimi kukusamehe, basi utakuwa umepoteza kabisa nafasi yako ya kusamehewa. Hivyo hatima yako haitakuwa juu bali chini. Kama huniamini basi kuwa jasiri na ufanye maovu, na kisha uone kile kitakachokupata. Kama wewe ni mtu mwenye ari anayetenda ukweli basi kwa hakika una fursa ya kusamehewa dhambi zako, na kiwango cha kutotii kwako kitakuwa kidogo zaidi na zaidi. Kama wewe ni mtu asiye radhi kutenda ukweli basi hakika dhambi zako mbele ya Mungu zitaongezeka, kiwango cha kutotii kwako kitakua zaidi na zaidi, mpaka wakati wa mwisho ambapo utakuwa umeangamia kabisa, na huo ndio wakati ambao ndoto yako ya kufurahisha ya kupokea baraka itaharibiwa. Usizichukulie dhambi zako kama makosa ya mtu asiye mkomavu au mpumbavu, usitumie kisingizio kwamba hukutenda ukweli kwa sababu ubora wako wa tabia ulio

duni ulifanya isiwezekane kuutenda, na hata zaidi, usizichukulie tu dhambi ulizofanya kama matendo ya mtu ambaye hakujua vizuri zaidi. Kama unajua vizuri kujisamehe na unajua vizuri kujitendea kwa ukarimu, basi Ninasema wewe ni mwoga ambaye kamwe hataupata ukweli, na dhambi zako kamwe hazitakoma kukusumbua, lakini zitakuzuia kuwahi kutosheleza madai ya ukweli na kukufanya milele kuwa mwenzi mwaminifu wa Shetani. Ushauri Wangu kwako bado ni: Usiwe makini sana kwa hatima yako tu na kutotilia maanani dhambi zako zilizofichika; zichukulie dhambi zako kwa makini, na usikose kutilia maanani dhambi zako zote kwa sababu ya kujali kuhusu hatima yako.

Ni Muhimu Sana Kuelewa Tabia ya Mungu

Kunayo mambo mengi ambayo Ninatumai mtaweza kufikia. Hata hivyo, matendo yenu na maisha yenu yote hayawezi kuridhisha matakwa Yangu kikamilifu, kwa hiyo lazima Niseme kile hasa ninachotaka kusema na kuwafafanulia mapenzi Yangu. Kwa kuwa utambuzi wenu ni ndogo na shukrani yenu pia ni ndogo, karibu mmekosa kabisa kujua tabia Yangu na dutu Yangu pia, na hivyo ni suala la dharura kwangu Mimi kuwafahamisha kuyahusu. Haijalishi hapo awali ulielewa kiwango kipi au kama uko radhi kujaribu kuelewa masuala haya, lazima bado Niyaeleeze kwenu kwa undani. Masuala haya si mageni kabisa kwenu, lakini inaonekana kwamba hamwelewi au hamjazoea maana iliyomo ndani yao. Wengi wenu mnao ufahamu dhaifu tu na aidha ufahamu kiasi na usiokamilika. Ili kuwasaidia kutenda ukweli kwa njia bora zaidi, yaani, kuweka maneno Yangu katika matendo kwa njia bora zaidi, Nafikiri kwamba ni masuala haya ambayo lazima kwanza myajue. Vinginevyo, imani yenu itabakia isiyo wazi, ya unafiki, na iliyopambwa sana na dini. Kama huelewi tabia ya Mungu, basi haitawezekana kwako kufanya kazi unayofaa kumfanyia. Kama hujui dutu ya Mungu, haitawezekana wewe kumwonyesha heshima na uchaji, lakini badala yake utakuwa tu mzembe asiyejali na kuepuka kusema ukweli wote, na zaidi, kukufuru kusikorekebisha. Ingawa kuelewa tabia ya Mungu kwa kweli ni muhimu sana, na maarifa ya dutu ya Mungu hayawezi kupuuzwa, hakuna yeyote amewahi kuchunguza kwa umakini au kudadisi masuala haya. Ni wazi kuona kwamba nyote mmepuzilia mbali amri za utawala Nilizozitoa. Kama hamuelewi tabia ya Mungu, basi mtaweza kukosea kwa urahisi sana tabia Yake. Kosa kama hilo ni sawa na kumkasirisha Mungu Mwenyewe, na tunda la msingi la tendo lako linakuwa ni kosa dhidi ya amri ya utawala. Sasa unafaa kutambua kwamba kuelewa tabia ya Mungu huja na kujua dutu Yake, nakwamba pamoja na kuelewa tabia ya Mungu huja kuelewa amri za utawala. Bila shaka, amri nyingi za utawala zinahusisha tabia ya Mungu, lakini tabia Yake haijaonyeshwa ndani yao kikamilifu. Kwa hivyo mnawahitaji kuongeza hatua nyingine katika kukuza ufahamu wenu wa tabia ya Mungu.

Ninaongea nanyi leo si katika hali ya mazungumzo ya kawaida, kwa hiyo lazima

myachukulie maneno Yangu kwa uangalifu na, zaidi, kuyatafakari kwa kina. Kile Ninachomaanisha na haya ni kwamba mmetoa jitihada ndogo sana kwa maneno ambayo Nimeyazungumza. Tunapokuja kwa tabia ya Mungu, hamko radhi hata zaidi kutafakari juu ya suala hili, na ni mara chache sana ambapo yeyote analiwekea juhudi. Kwa hiyo, Nasema kwamba imani yenu ni mazungumzo ya kujionyesha tu. Hata sasa, hakuna hata mmoja wenu ametoa jitihada yoyote ya dhati kwa udhaifu wenu mkuu zaidi. Mmenisikitisha baada ya maumivu yote Niliyoyapitia kwa ajili yenu. Si ajabu kwamba hammjali Mungu na mnaishi maisha yasiyo na ukweli. Ni vipi watu kama hawa wanaweza kuchukuliwa kama watakatifu? Sheria ya mbinguni haitavumilia kitu kama hiki! Kwa sababu mnao uelewa mdogo sana wa hili, basi itabidi Nitumie pumzi zaidi.

Tabia ya Mungu ni mada ambayo inaonekana kuwa ya dhahania sana kwa kila mtu na aidha ambayo haikubaliwi kwa urahisi, kwani tabia Yake ni tofauti na hulka ya binadamu. Mungu, vilevile, anazo hisia za raha, hasira, huzuni, na furaha, lakini hisia hizo zinatofautiana na zile za binadamu. Mungu ndicho kile Alichu na Anacho kile anacho. Kila kitu Anachokidhihirisha na kukifichua ni viwakilishi vya dutu Yake na utambulisho Wake. Kila alichu na anacho, pamoja na dutu na utambulisho Wake vyote ni vitu ambavyo haviwezi kubadilishwa na binadamu yeyote. Tabia Yake inajumuisha upendo Wake kwa binadamu, tulizo kwa binadamu, chuki kwa binadamu, na hata zaidi, uelewa wa kina wa binadamu. Hulka ya binadamu, hata hivyo, inaweza kuwa yenye matumaini mema, changamfu, au ngumu. Tabia ya Mungu ni ile ambayo inamilikiwa na Mtawala wa vitu vyote na viumbe vyote vyenye uhai, kwa Bwana wa viumbe vyote. Tabia Yake inawakilisha heshima, nguvu, uadilifu, ukubwa, na zaidi kuliko vyote, mamlaka ya juu kabisa. Tabia Yake ni ishara ya mamlaka, ishara ya kila kitu kilicho cha haki, cha kuvutia, ishara ya kila kitu kilicho chema na kizuri. Aidha, ni ishara ya Yeye ambaye hawezi^[a] kushindwa au kushambuliwa na giza na nguvu yoyote ya adui, pamoja na ishara ya Yeye ambaye hawezi kukosewa (wala Hatavumilia kukosewa)^[b] na kiumbe yeyote aliyeumbwa. Tabia Yake ni ishara ya nguvu za kiwango cha juu zaidi. Hakuna mtu au watu wanao uwezo au wanaoweza kutatiza kazi Yake au tabia Yake. Lakini hulka ya binadamu ni ishara tu ya mamlaka kidogo ya binadamu juu ya wanyama. Binadamu mwenyewe hana mamlaka, hana uhuru, na hana uwezo wa kuzidi nafsi, bali katika dutu yake ni yule ambaye kwa woga yuko chini ya watu, matukio na mambo ya kila aina. Raha ya Mungu inatokana na uwepo na kuibuka kwa haki na mwangaza; kwa sababu ya kuangamizwa kwa giza na maovu. Anafurahia kwa sababu Ameuleta mwangaza na maisha mazuri kwa wanadamu; raha Yake ni raha ya haki, ishara ya uwepo wa kila kitu kilicho kizuri, na zaidi, ishara ya fadhili. Hasira ya Mungu inatokana na uharibifu ambao kuwepo na kuingilia kwa dhuluma kunaleta kwa wanadamu Wake, kwa sababu ya uwepo wa maovu na giza, kwa sababu ya uwepo wa vitu vinavyoondoa ukweli, na hata zaidi kwa

sababu ya uwepo wa vitu vinavyopinga kile ambacho ni kizuri na chema. Hasira Yake ni ishara ya kwamba vitu vyote vibaya havipo tena, na fauka ya hayo, ni ishara ya utakatifu Wake. Huzuni Yake ni kwa sababu ya wanadamu, ambao Amekuwa na matumaini nao lakini ambao wameanguka katika giza, kwa sababu kazi Afanyayo kwa mwanadamu haifikii matarajio Yake, na kwa sababu binadamu Awapendao hawawezi wote kuishi katika mwanga. Anahisi huzuni kwa sababu ya wanadamu wasio na hatia, kwa yule binadamu mwaminifu lakini asiyejua, na kwa yule mwanadamu mzuri lakini mwenye upungufu katika maoni yake mwenyewe. Huzuni Yake ni ishara ya wema Wake na huruma Yake, ishara ya uzuri na ukarimu. Furaha yake, bila shaka, inatokana na kuwashinda adui Zake na kupata imani nzuri ya binadamu. Aidha, inatokana na kuondolewa na kuangamizwa kwa nguvu zote za adui na kwa sababu wanadamu hupokea maisha mazuri na yenye amani. Furaha ya Mungu ni tofauti na raha ya binadamu; badala yake, ni ile hisia ya kupokea matunda mazuri, hisia ambayo ni kubwa zaidi kuliko raha. Furaha Yake ni ishara ya wanadamu kuwa huru dhidi ya mateso kutoka wakati huu kuendelea, na ishara ya wanadamu kuingia katika ulimwengu wa mwangaza. Hisia za mwanadamu, kwa upande mwingine, zote huibuka kwa ajili ya masilahi yake mwenyewe, na wala si kwa ajili ya haki, mwangaza, au kile ambacho ni cha kupendeza, sembuse neema inayotolewa na Mbinguni. Hisia za wanadamu ni za ubinafsi na zinamilikiwa na ulimwengu wa giza. Hisia hizo hazipo kwa ajili ya mapenzi, sembuse mpango wa Mungu, na kwa hiyo mwanadamu na Mungu hawawezi kamwe kuzungumziwa hapohapo. Mungu siku zote anayo mamlaka ya juu zaidi na ni mwenye heshima kila wakati, ilhali mwanadamu siku zote ni wa chini, siku zote asiye na thamani. Hii ni kwa sababu Mungu siku zote anajitolea mhanga na kujitoa Mwenyewe kwa wanadamu; mwanadamu, hata hivyo, siku zote huchukua na kujitahidi kwa ajili yake pekee. Siku zote Mungu anashughulikia kwa dhati kuendelea kuishi kwa wanadamu, ilhali mwanadamu kamwe hachangii kitu kwa ajili ya mwangaza au haki. Hata kama mwanadamu anajitahidi sana kwa muda, ni dhaifu sana kiasi cha kutoweza kustahimili dhoruba hata kidogo, kwani jitihada za mwanadamu siku zote ni kwa ajili yake mwenyewe na wala si kwa ajili ya wengine. Mwanadamu siku zote ni mbinafsi, huku naye Mungu siku zote si mwenye ubinafsi. Mungu ndiye chanzo cha vyote vilivyo vya haki, vyema, na vya uzuri, huku naye mwanadamu ni yule anayerithi na kudhihirisha vyote vyenye sura mbaya na vyenye maovu. Mungu hatawahi kubadilisha dutu Yake ya haki na uzuri, ilhali mwanadamu anaweza kabisa, wakati wowote, kusaliti haki na kupotoka kutoka kwa Mungu.

Kila sentensi Niliyoizungumza ina tabia ya Mungu ndani yake. Mngefanya vizuri endapo mngetafakari kuhusu maneno Yangu kwa umakini, na kwa kweli mtafaidi pakubwa kutoka kwa maneno hayo. Dutu ya Mungu ni ngumu sana kuelewa, lakini Ninaamini kwamba nyinyi nyote mnayo angalau mawazo fulani kuhusu tabia ya Mungu. Ninatumai, basi, kwamba mtanionyesha

Mimi na kufanya mengi zaidi ya yale ambayo hayakosei tabia ya Mungu. Kisha Nitatulizwa moyo. Kwa mfano, mweke Mungu katika moyo wako siku zote. Unapochukua hatua, fanya hivyo kulingana na maneno Yake. Tafuta nia Zake katika kila kitu, na usifanye kile ambacho kitavunjia heshima na kumdhalilisha Mungu. Hata zaidi usimweke Mungu nyuma ya akili zako ili ukajaze uwazi wa baadaye katika moyo wako. Ukifanya hivyo, basi utakuwa umekosea tabia ya Mungu. Tena, tuchukulie kwamba kamwe hutamki matamshi ya kukufuru au kulalamika dhidi ya Mungu maisha yako yote, na tena, tuchukulie kwamba unaweza kufanya kikamilifu kila kitu ambacho amekuaminia wewe na pia kutii maneno Yake yote katika maisha yako yote, basi utakuwa umeweza kuepuka kwa kukosea amri za utawala. Kwa mfano, kama umewahi kusema “Kwa nini sifikirii kwamba Yeye ni Mungu?” “Nafikiri kwamba maneno haya ni nuru kiasi ya Roho Mtakatifu tu,” “Katika maoni yangu, si kila kitu ambacho Mungu anakifanya lazima ni sahihi,” “Ubinadamu wa Mungu hauna ukubwa zaidi kuliko wangu,” “Maneno ya Mungu hayaaminiki kabisa,” au matamshi mengine kama hayo ya kuhukumu, basi Nakusihi wewe kukiri na kutubu dhambi zako mara nyingi zaidi. Vinginevyo, hutawahi kuwa na fursa ya msamaha, kwani hukosei mwanadamu, ila Mungu Mwenyewe. Unaweza kuamini kwamba wewe unamhukumu mtu tu, lakini Roho wa Mungu haichukulii hivyo. Wewe kutoheshimu mwili Wake ni sawa na kumvunjia Yeye heshima. Kama hali ni hivi, basi si ni kweli kwamba umekosea tabia ya Mungu? Lazima ukumbuke kwamba kila kitu kinachofanywa na Roho wa Mungu kinafanywa ili kukinga kazi Yake katika mwili na ili kazi hii ifanywe vizuri. Ukiyapuuza haya, basi Nasema kwamba wewe ni mtu ambaye kamwe hataweza kufaulu katika kumwamini Mungu. Kwani umechochea hasira ya Mungu, kwa hivyo Atatumia adhabu inayofaa ili kukufunza adabu.

Kupata kujua dutu ya Mungu si jambo dogo. Lazima uelewe tabia Yake. Katika njia hii, polepole na bila kujua, utanza kujua dutu ya Mungu. Wakati umeingia katika maarifa haya, utajipata ukisonga mbele hadi kwa hali iliyo ya juu na ya kupendeza zaidi. Hatimaye, utaaibika kutokana na nafsi yako ya kuchukiza, kiasi kwamba unahisi hakuna mahali pa kujificha. Wakati huo, kutakuwa na machache zaidi na zaidi katika mwenendo wako ya kukosea tabia ya Mungu, moyo wako utakuwa karibu zaidi na zaidi na ule wa Mungu, na polepole upendo wako Kwake utakua ndani ya moyo wako. Hii ni ishara ya wanadamu kuingia katika hali nzuri. Lakini kufikia sasa bado hamjapata hili. Mnaposhughulika huku na kule kwa ajili ya majaaliwa yenu, ni nani angefikiria kujaribu kujua dutu ya Mungu? Kama hali hii itaendelea, nyinyi mtazikosea amri za utawala bila kujua, kwani mnaifahamu kidogo sana kuhusu tabia ya Mungu. Kwa hivyo, kile mfanyacho sasa hakiweki msingi wa makosa yenu dhidi ya tabia ya Mungu? Kwamba Ninawaomba muelewe tabia ya Mungu haipingani na kazi Yangu. Kwani mkikosea amri za utawala mara nyingi, basi ni nani kati yenu anayeweza kutoroka adhabu? Je, basi kazi Yangu haingekuwa bure kabisa? Kwa hivyo, Ningali Naomba kwamba, pamoja na kuchunguza

mienendo yenu binafsi, muwe waangalifu zaidi na hatua mnazochukua. Haya ndiyo yatakuwa mahitaji ya juu zaidi nitakayowaomba, na Ninatumai kwamba nyote mtayafikiria kwa umakini na kuyaona kuwa muhimu kabisa. Endapo siku ifike ambapo matendo yenu yatanichochea Mimi hadi kuwa katika hali iliyojaa hasira, basi matokeo yatakuwa yenu pekee kufikiria, na hakutakuwa na mwingine yeyote atakayevumilia adhabu hiyo kwa niaba yenu.

Tanbihi:

a. Maandishi asilia yanasema “ni ishara ya kutoweza.”

b. Maandishi asilia yanasema “na vilevile ishara ya kutoweza kukosewa kuwa (na kutovumilia kukosewa).”

Jinsi ya Kumjua Mungu Duniani

Nyinyi nyote mna furaha kupokea tuzo mbele ya Mungu na kuwa walengwa wa fadhili Zake machoni Pake. Haya ni matakwa ya kila mtu baada ya yeye kuanza kuwa na imani kwa Mungu, kwani mwanadamu kwa moyo wake wote hujitahidi kupata mambo yaliyo juu na hakuna aliye tayari kubaki nyuma ya wengine. Hii ndiyo njia ya mwanadamu. Kwa sababu hii hasa, wengi kati yenu wanajaribu daima kujipendekeza kwa Mungu mbinguni, lakini kwa kweli, uaminifu wenu na uwazi kwa Mungu ni wa kiasi kidogo sana ukilinganishwa na uaminifu na uwazi wenu kwenu wenyewe. Mbona Nasema hivi? Kwa sababu Sikiri uaminifu wenu kwa Mungu kabisa, na zaidi Nakana kuwepo kwa Mungu aliye ndani ya mioyo yenu. Hiyo ni kusema, Mungu mnayemwabudu, Mungu asiye dhahiri mnayempenda, hayupo kabisa. Kinachonifanya niseme haya kwa uhakika ni kwamba mko mbali sana na Mungu wa kweli. Uaminifu mnaomiliki unatokana na kuwepo kwa sanamu mioyoni mwenu, na kunihusu Mimi, Mungu anayeonekana kama asiye mkubwa wala mdogo machoni penu, mnachofanya ni kunikiri kwa maneno tu. Ninaposema juu ya umbali wenu mkubwa kutoka kwa Mungu, Ninamaanisha jinsi mlivyo mbali sana na Mungu wa kweli, ilhali Mungu asiye dhahiri Anaonekana kuwa karibu. Nisemapo “asiye mkubwa,” inamaanisha jinsi Mungu mnayemwamini siku ya leo anaonekana tu kuwa mwanadamu asiye na uwezo mkubwa; mwanadamu asiye wa fahari sana. Na Nisemapo, “asiye mdogo,” inamaanisha kuwa ingawa mwanadamu huyu hawezi kuita upepo na kuamuru mvua, hata hivyo Anaweza kumwita Roho wa Mungu kufanya kazi inayotingisha mbingu na dunia, hivyo kumchanganya mwanadamu kabisa. Kwa nje, nyote mnaonekana kuwa watiifu sana kwa huyu Kristo aliye duniani, lakini kwa kiini hamna imani Kwake wala kumpenda. Ninachomaanisha ni kwamba yule mliye na imani kwake kwa kweli ni yule Mungu asiye dhahiri katika hisia zenu, na yule kweli mnayempenda ni Mungu mnayemtamani usiku na mchana, lakini bado hamjamwona kamwe kibinafsi. Na kuhusu huyu Kristo, imani yenu ni sehemu tu, na upendo wenu Kwake si kitu. Imani inamaanisha imani na kusadiki; upendo unamaanisha kusujudu na kusifu ndani ya mioyo yenu, bila kuondoka. Lakini imani yenu na

upendo wenu kwa Kristo wa siku ya leo vimepunguka chini ya hili. Ikujapo kwa imani, mna imani Kwake jinsi gani? Ikujapo kwa upendo, mnampenda jinsi gani? Hamjui kabisa kuhusu tabia Yake, sembuse kiini Chake, hivyo ni jinsi gani kwamba mna imani Kwake? Uko wapi uhalisi wa imani yenu Kwake? Mnampenda jinsi gani? Uko wapi uhalisi wa upendo wenu Kwake?

Wengi wamenifuata bila kusita hadi leo, na katika miaka hii michache, nyote mmepitia uchovu mwingi. Nimefahamu vizuri tabia ya asili na mazoea ya kila mmoja wenu, na imekuwa vigumu sana kuingiliana nanyi. Cha kusikitisha ni kwamba ingawa nina maarifa nyingi kuwahusu, hamna ufahamu hata kidogo kunihusu. Sio ajabu wengine wanasema mlidanganywa na mwanadamu katika wakati wa mkanganyiko. Hakika, hamwelewi chochote kuhusu tabia Yangu, na hata zaidi hamwezi kufahamu yaliyo akilini Mwangu. Sasa ninyi kunielewa visivyo kunaongezeka haraka, na imani yenu Kwangu inabaki ile imani iliyokanganyika. Badala ya kusema kwamba mna imani na Mimi, ingekuwa bora kusema kwamba nyote mnajaribu kujipendekeza Kwangu na kunibembeleza. Nia zenu ni rahisi sana—yeyote anayeweza kunituza, nitamfuata, na yeyote anayeweza kuniwezesha kutoroka majanga makubwa, nitaamini kwake, awe Mungu ama Mungu fulani yeyote. Hakuna kati ya haya yanayonihusu. Kuna wanadamu wengi kama hao kati yenu, na hali hii ni nzito sana. Ikiwa siku moja, majaribio yatafanywa kuona ni wangapi kati yenu wanamwamini Kristo kwa sababu mna umaizi kuhusu kiini Chake, basi Nahofia kwamba hakuna mmoja wenu atakuwa na uwezo kufanya Ninavyotaka. Hivyo haitakuwa hoja kwa kila mmoja wenu kuzingatia swali hili: Mungu mliye na imani na Yeye ni tofauti sana na Mimi, na kwa hivyo, nini basi ni kiini cha imani yenu kwa Mungu? Kadri mnavyozidi kuamini katika mnayedai kuwa Mungu wenu, ndivyo mnavyozidi kupotea mbali sana nami. Basi, ni nini msingi wa suala hili? Nina uhakika hakuna mmoja wenu amewahi kufikiria suala hili, lakini mmefikiria uzito wake? Mmewaza kuhusu matokeo ya kuendelea na imani ya namna hii?

Sasa, matatizo yaliyowekwa mbele yenu ni mengi, na hakuna mmoja wenu aliye na uhodari wa kuleta ufumbuzi. Iwapo haya yataendelea, basi walio katika hatari ya kupoteza ni nyinyi wenyewe pekee. Nitawasaidia kuyatambua matatizo, lakini itabakia kwenu kupata ufumbuzi.

Nawathamini sana wale wasio na shaka kuhusu wengine na pia nawapenda sana wale wanaokubali ukweli kwa urahisi; kwa aina hizi mbili za wanadamu Ninaonyesha utunzaji mkubwa, kwani machoni Pangu wao ni waaminifu. Kama una udanganyifu mwingi, basi utakuwa na moyo wenye hadhari na mawazo ya shaka juu ya mambo yote na wanadamu wote. Kwa sababu hii, imani yako Kwangu inajengwa kwa msingi wa shaka. Imani kama hii ni moja ambayo kamwe Sitaitambua. Bila imani ya kweli, basi utakuwa mbali hata zaidi na upendo wa

kweli. Na ikiwa unaweza kumshuku Mungu na kumkisia utakavyo, basi wewe bila shaka ni mdanganyifu zaidi kati ya wanadamu wengine. Mnakisia iwapo Mungu anaweza kuwa kama mwanadamu: mwenye dhambi isiyosameheka, mwenye tabia ndogondogo, anayependelea na asiye na mantiki, aliyekosa hisia ya haki, mwenye mbinu ovu, mdanganyifu na mjanja, na pia anayefurahishwa na uovu na giza, na kadhalika. Si sababu ambayo mwanadamu ana mawazo kama haya kwamba hana hata ufahamu mdogo wa Mungu? Imani kama hii ni sawa na dhambi! Zaidi ya hayo, kuna hata wale wanaoamini kwamba Sifurahishwi na yeyote isipokuwa wale wanaojirairai na kujipendekeza, na kwamba wale wasio na ujuzi huu hawatakaribishwa na watapoteza nafasi yao katika nyumba ya Mungu. Je, haya ndiyo maarifa ambayo mmepata kwa miaka hii yote mingi? Ni haya ndiyo mliyoyapata? Na ufahamu wenu kunihusu hauko kwa kutoelewa kama huku tu; mbaya hata zaidi ni kukufuru kwenu Roho wa Mungu na kuitukana Mbingu. Hii ndiyo maana Ninasema kwamba imani kama yenu itawasababisha tu kupotea mbali na Mimi na kukuwa na upinzani mkubwa dhidi Yangu. Kwa miaka mingi ya kazi, mmeona ukweli mwingi, lakini mnajua kile masikio Yangu yamesikia? Ni wangapi kati yenu walio tayari kukubali ukweli? Nyote mnaamini kwamba mko tayari kulipa gharama ya ukweli, lakini ni wangapi walioteseka kweli kwa ajili ya ukweli? Yote yaliyo ndani ya mioyo yenu ni uovu, na hivyo mnaamini kwamba yeyote, bila kujali ni nani, ni mjanja na asiye mwaminifu. Hata mnaamini kwamba Mungu mwenye mwili angekuwa bila moyo wa ukarimu na upendo wema kama tu binadamu wa kawaida. Zaidi ya hayo, mnaamini kwamba tabia ya adabu na asili yenye huruma na ukarimu ziko kwa Mungu wa mbinguni pekee. Na mnaamini kwamba mtakatifu kama huyu hayuko, na kwamba giza na uovu tu ndio unaotawala duniani, ilhali Mungu ni kitu ambacho mwanadamu huwekea matumaini yake ya mazuri na mema, na mtu maarufu aliyebuniwa na mwanadamu. Ndani ya akili zenu, Mungu aliye mbinguni ni mnyoofu sana, mwenye haki, na mkubwa, anayestahili ibada na upendezewaji, lakini Mungu huyu aliye duniani ni mbadala tu na chombo cha Mungu aliye mbinguni. Mnaamini Mungu huyu hawezi kuwa sawa na Mungu wa mbinguni, na hata zaidi hawezi kutajwa kwa pumzi moja na Yeye. Ifikapo kwa ukubwa na heshima ya Mungu, ni mali ya utukufu wa Mungu aliye mbinguni, lakini ifikapo kwa tabia na upotovu wa mwanadamu, vinahusishwa na Mungu aliye duniani. Mungu aliye mbinguni daima ni mkuu, ilhali Mungu wa duniani daima ni asiye na maana, mdhaifu na asiyejimudu. Mungu aliye mbinguni haathiriwi na hisia, kwa haki tu, ilhali Mungu aliye duniani ana motisha za kibinafsi tu na Hana haki na mantiki yoyote. Mungu aliye mbinguni hana udanganyifu hata kidogo na daima ni mwaminifu, ilhali Mungu wa duniani daima ana upande mdanganyifu. Mungu aliye mbinguni anampenda sana mwanadamu, ilhali Mungu wa duniani anamjali mwanadamu isivyotosha, hata kumpuuza kabisa. Ufahamu huu usio sahihi umewekwa kwa muda mrefu kwa mioyo yenu na unaweza pia kuendelezwa mbele katika siku za usoni. Mnachukulia matendo yote ya Kristo kwa msimamo wa wadhalimu na kuhukumu kazi Yake

yote na utambulisho Wake na kiini Chake kwa mtazamo wa waovu. Mmefanya kosa kubwa sana na kufanya kile ambacho hakijawahi kufanywa na wale kabla yenu. Yaani, mnamtumikia tu Mungu mkuu aliye mbinguni na taji juu ya kichwa Chake na hamshughulikii kamwe Mungu mnayemchukulia kuwa asiye na maana kabisa kiasi cha kutoonekana kwenu. Hii siyo dhambi yenu? Huu sio mfano halisi wa kosa lenu dhidi ya tabia ya Mungu? Mnamwabudu sana Mungu aliye mbinguni. Mnapenda sana sura zilizo kuu na kuheshimu wanaojulikana kwa ajili ya umbuji wao. Mnaamrisha kwa furaha na Mungu Anayejaza mikono yenu na utajiri, na mnatamani sana Mungu Anayeweza kutimiza tamaa zenu zote. Yule tu msiyemwabudu ni Mungu huyu asiye mkuu; Chombo chenu tu cha chuki ni ushirikiano na huyu Mungu ambaye hakuna mwanadamu anayeweza kumchukulia kuwa mkuu. Kitu pekee ambacho hamko tayari kufanya ni kumtumikia huyu Mungu ambaye hajawahi kuwapa senti hata moja, na Yule tu msiyemtamani ni huyu Mungu asiyependeza. Mungu kama huyu hawezi kuwawezesha kupanua upeo wenu wa macho, kuhisi kana kwamba mmepata hazina, sembuse kutimiza mnachotaka. Mbona, basi, mnamfuata? Je, mmefikiria kuhusu maswali kama haya? Kile ufanyacho hakimkosei huyu Kristo tu; cha muhimu hata zaidi, kinakosea Mungu aliye mbinguni. Nadhani kwamba, haya siyo madhumuni ya imani yenu kwa Mungu!

Mnatamani sana kwa Mungu kufurahishwa nanyi, lakini bado mko mbali sana na Mungu. Tatizo ni nini hapa? Mnakubali tu maneno Yake, lakini sio ushughulikiaji na upogoaji Wake; hata zaidi hamwezi kukubali mpangilio Wake wote, kuwa na imani kamilifu Kwake. Tatizo, basi, ni gani hapa? Kimsingi, imani yenu ni kaka tupu la yai lisiloweza kutoa kifaranga. Kwani imani yenu haijawaletae ukweli ama kuwapa maisha, na badala imewaletae hisia danganyifu ya tumaini na msaada. Madhumuni ya imani yenu kwa Mungu ni kwa ajili ya tumaini hili na msaada huu badala ya ukweli na maisha. Kwa hivyo, Nasema kwamba mkondo wa imani yenu kwa Mungu si mwingine bali ni kujaribu kujipendekeza kwa Mungu kupitia utumwa na kutokuwa na aibu, na hauwezi kuchukuliwa kuwa imani ya kweli hata kidogo. Kifaranga anaweza kujitokezaje kwa imani kama hii? Kwa maneno mengine, ni tunda lipi ambalo imani kama hii inaweza kuzalisha? Azma ya imani yenu kwa Mungu ni kutimiza nia zenu kupitia kumtumia Mungu. Huu sio ukweli zaidi unaoonyesha kosa lenu dhidi ya tabia ya Mungu? Mnaamini kuwepo kwa Mungu aliye mbinguni lakini mnakataa yule Mungu aliye duniani. Hata hivyo, Sikubaliani na maoni yenu. Nawapongeza tu wale wanadamu wanaosimama imara na kumtumikia Mungu wa duniani, kamwe sio wale wasiomkiri Kristo aliye duniani. Bila kujali jinsi wanadamu kama hawa walivyo waaminifu kwa Mungu aliye mbinguni, mwishowe, hawatauepuka mkono Wangu unaoadhibu waovu. Wanadamu kama hawa ni waovu; ni wale waovu wanaompinga Mungu na hawajawahi kumtii Kristo kwa furaha. Bila shaka, idadi yao inajumuisha wale wote wasiomjua na, zaidi, wasiomkiri Kristo. Unaamini kwamba unaweza

kutenda utakavyo kwa Kristo alimradi wewe ni mwaminifu kwa Mungu aliye mbinguni? Makosa! Kutomjua Kristo kwako ni kutomjua Mungu aliye mbinguni. Bila kujali uaminifu wako kwa Mungu aliye mbinguni, ni maneno matupu tu na kujifanya, kwani Mungu aliye duniani si muhimu tu kwa mwanadamu kupokea ukweli na ufahamu mkubwa zaidi, lakini hata zaidi ni muhimu kwa lawama ya mwanadamu na baadaye kwa kuushika ukweli kuwaadhibu waovu. Umeelewa matokeo yenye faida na yanayodhuru hapa? Umepata kuyapitia? Ningependa siku moja hivi karibuni ninyi muelewe ukweli huu: Kumjua Mungu, mnapaswa kumjua sio tu Mungu wa mbinguni lakini, hata muhimu zaidi, Mungu aliye duniani. Msiyachanganye yaliyo kipaumbele ama kuruhusu yaliyo ya pili kuchukua nafasi ya yaliyo ya msingi. Ni kwa njia hii tu ndiyo unaweza kujenga uhusiano mzuri na Mungu, kuwa karibu na Mungu, na kupeleka moyo wako karibu na Yeye. Kama umekuwa wa imani kwa miaka nyingi na kushirikiana na Mimi kwa muda mrefu, lakini bado unabaki mbali na Mimi, basi Nasema kwamba ni lazima iwe kuwa mara nyingi unaikosea tabia ya Mungu, na mwisho wako utakuwa mgumu sana kufikiria. Kama miaka mingi ya ushirikiano na Mimi haijakubadilisha kuwa mwanadamu aliye na ubinadamu na ukweli, ila badala yake imeingiza njia zako ovu ndani ya asili yako, na huna maono maradufu ya uwongo kuhusu fahari kuliko awali pekee lakini kutonielewa kwako kumeongezeka pia, kiasi kwamba unakuja kunichukulia kuwa rafiki yako mdogo wa kando, basi Nasema kwamba mateso yako si ya juujuu tena, lakini yamepenya ndani kwa mifupa yako. Yote yaliyosalia ni wewe kusubiri matayarisho ya mazishi yako kufanywa. Huhitaji kunisihi basi Niwe Mungu wako, kwani umetenda dhambi inayostahili kifo, dhambi isiyosameheka. Hata kama Ningeweza kuwa na huruma nawe, Mungu aliye mbinguni Atasisitiza kuchukua maisha yako, kwani kosa lako dhidi ya tabia ya Mungu si shida ya kawaida, lakini lile lililo kubwa sana kiasili. Wakati utakapofika, usinilaumu kwa sababu ya kutokujulisha mbeleni. Yote yanarudia haya: Wakati unashirikiana na Kristo—Mungu aliye duniani—kama mwanadamu wa kawaida, yaani, unapoamini kwamba Mungu huyu si chochote ila ni mwanadamu, ni hapo basi ndipo utaangamia. Hili ndilo onyo Langu la pekee kwenu nyinyi nyote.

Tatizo Zito Sana: Usaliti (1)

Kazi Yangu iko karibu kukamilika. Miaka mingi ambayo tumeshinda pamoja imekuwa kumbukumbu zisizovumilika za siku za nyuma. Nimeendelea kurudia maneno Yangu na Sijakoma kuendelea katika kazi Yangu mpya. Bila shaka, ushauri Wangu ni sehemu muhimu katika kila sehemu ya kazi Ninayoifanya. Bila ushauri Wangu, ninyi nyote mtapotea, na kuchanganyikiwa hata zaidi. Kazi Yangu sasa karibu inakamilika na kuisha; bado Nataka kufanya kazi fulani katika kutoa ushauri, hiyo ni, kutoa baadhi ya maneno ya ushauri ili muyasikilize. Natumai tu kwamba hamtapoteza juhudi Zangu zenye kujitahidi na zaidi ya hayo, kwamba mnaweza kuelewa utunzaji wote na fikira ambazo Nimetumia, mkiyachukulia maneno

Yangu kama msingi wa jinsi mnavyotenda kama binadamu. Iwe ni maneno ambayo mko tayari kuyasikiliza au la, iwe ni maneno ambayo mnafurahia kuyakubali au mnayakubali bila raha, lazima muyachukulie kwa uzito. Vinginevyo, tabia na mielekeo yenu isiyokuwa ya kujali itanifadhaisha Mimi kweli na hata zaidi, kuniudhi. Natumai sana kwamba nyote mnaweza kuyasoma maneno Yangu tena na tena—mara elfu kadhaa—na hata kuyakariri. Ni kwa namna hiyo tu ndiyo hamtayaacha matarajio Yangu kwa ajili yenu. Hata hivyo, hakuna hata mmoja wenu anayeishi hivi sasa. Hata, nyote mmezama katika maisha fisadi ya kula na kunywa hadi kushiba, na hakuna yeyote kati yenu anayeyatumia maneno Yangu kuusitawisha moyo na nafsi yake. Kwa sababu hii ndiyo Nimehitimisha kuhusu uso wa kweli wa mwanadamu: Mwandamu anayeweza kunisaliti wakati wowote, na hakuna yeyote anayeweza kuwa mwaminifu kabisa kwa maneno Yangu.

“Mwanadamu amepotoshwa sana na Shetani kiasi kwamba hana sura ya mwanadamu tena.” Usemi huu sasa umepata utambuzi kidogo kutoka kwa idadi kubwa ya watu. Inasemwa hivyo kwa sababu “utambuzi” hapa ni kukiri juu juu tu kinyume na maarifa ya kweli. Kwa kuwa hakuna yeyote kati yenu anayeweza kujitathmini kwa usahihi wala kujichanganua kabisa, daima mnaamini nunu nusu, mnayashuku maneno Yangu nusu nusu. Lakini wakati huu Nautumia ukweli kuelezea tatizo kubwa zaidi mlio nalo, na hilo ni usaliti. Nyote mnao uzoefu wa neno “usaliti” kwa sababu watu wengi wamefanya kitu kuwasaliti wengine awali, kama vile mume kumsaliti mke wake, mke kumsaliti mume wake, mwana kumsaliti baba yake, binti kumsaliti mama yake, mtumwa kumsaliti bwana wake, marafiki kusalitiana, jamaa kusalitiana, wauzaji kuwasaliti wanunuzi, na mengineyo. Mifano hii yote ina asili ya usaliti. Kwa kifupi, usaliti ni aina ya tabia ambayo mtu huvunja ahadi, hukiuka kanuni za maadili, au huenda dhidi ya maadili ya kibinadamu, na ambayo huonyesha kupoteza ubinadamu. Kama mwanadamu, bila kujali kama unakumbuka iwapo umewahi kufanya kitu cha kumsaliti mwingine au ikiwa tayari umewasaliti wengine mara nyingi, kuzungumza kwa ujumla, kama ninyi mmezaliwa katika dunia hii basi mmefanya kitu kuusaliti ukweli. Kama una uwezo wa kuwasaliti wazazi au marafiki basi una uwezo wa kuwasaliti wengine, na zaidi ya hayo una uwezo wa kunisaliti Mimi na kufanya mambo ambayo Ninayadharau. Kwa maneno mengine, usaliti si aina ya utovu wa maadili tu kwa nje, lakini ni kitu ambacho hakikubaliani na ukweli. Aina hii ya kitu hasa ni chanzo cha upinzani wa mwanadamu na uasi kuhusiana na Mimi. Hii ndio sababu Nimeufupisha katika maelezo yafuatayo: Usaliti ni asili ya mwanadamu. Asili hii ni adui wa kimaumbile wa kila mtu kuwa sambamba na Mimi.

Tabia ambayo haiwezi kunitii kabisa ni usaliti. Mwenendo ambao hauwezi kuwa mwaminifu Kwangu ni usaliti. Kunidanganya na kutumia uongo kunilaghai ni usaliti. Kujawa na dhana na kuzieneza kila mahali ni usaliti. Kutozilinda shuhuda na maslahi Yangu ni usaliti.

Kubuni tabasamu wakati mtu ameniacha moyoni mwake ni usaliti. Tabia hizi ni mambo yote ambayo daima mna uwezo wa kuyafanya, na pia ni za kawaida kati yenu. Hakuna mmoja wenu anayeweza kufikiri kwamba hilo ni tatizo, lakini Mimi sifikirii hivyo. Siwezi kuchukulia kunisaliti kama jambo dogo, na zaidi ya hayo siwezi kulipuuza. Sasa, Nafanyapo kazi miongoni mwenu, mnakuwa wenye tabia ya aina hii—ijapo siku ile ambapo hakutakuwa na mtu wa kuwalinda, hamtakuwa kama wezi waliojitangaza kuwa wafalme? Wakati hili linafanyika na mnasababisha janga kubwa, nani atakuwa hapa kuvisafisha vitu tena na kuondoa uchafu? Mnaweza kufikiri kwamba baadhi ya vitendo vya usaliti ni kitu cha mara moja tu badala ya tabia ya kuendelea, na hakipaswi kutajwa kwa uzito hivi, kikiwasababisha kuadhirika. Kama kweli mnaamini hivyo, basi mnakosa wepesi wa kuhisi. Kadiri mtu anavyofikiri hivi, ndivyo anavyokuwa kielelezo na umboasili wa uasi. Asili ya mtu ni maisha yake, ni kanuni ambayo anaitegemea ili kuendelea kuishi, na anashindwa kuibadilisha. Jinsi ilivyo hali ya usaliti—kama unaweza kufanya kitu ili kumsaliti ndugu au rafiki, hii inathibitisha kwamba ni sehemu ya maisha yako na hali ambayo ulizaliwa nayo. Hiki ni kitu ambacho hakuna mtu anaweza kukikana. Kwa mfano, kama mtu anapenda kuiba vitu vya watu wengine, basi hii “kupenda kuiba” ni sehemu ya maisha yake. Ni kwamba tu wakati mwingine anaiba, na wakati mwingine haibi. Bila kujali kama anaiba au la, haiwezi kuthibitisha kwamba kuiba kwake ni aina ya tabia. Badala yake, inathibitisha kwamba kuiba kwake ni sehemu ya maisha yake, yaani, asili yake. Baadhi ya watu watauliza: Kwa kuwa ni asili yake, basi kwa nini wakati mwingine anaona vitu vizuri lakini haviibi? Jibu ni rahisi sana. Kuna sababu nyingi kwa nini haibi, kama vile kama bidhaa ni kubwa mno kwake kuinyakua akitazamwa na watu, au hakuna wakati mzuri wa kutenda, au bidhaa ni ghali sana, imelindwa vikali, au hana nia hasa ya kitu kizuri kama hicho, au bado hajafikiria matumizi ya kitu hicho, na mengineyo. Sababu hizi zote zinawezekana. Lakini haidhuru, akikiiba au la, hii haiwezi kuthibitisha kuwa hiyo dhana humjia akilini kwa muda tu. Kinyume chake, hii ni sehemu ya asili yake ambayo ni ngumu kuirudia tena. Mtu kama huyo haridhiki na kuiba mara moja tu, lakini mawazo ya kudai vitu vya wengine kama vyake huamshwa wakati wowote anapokutana na kitu kizuri au hali inayofaa. Hii ndiyo sababu Nasema kwamba wazo hili haliinuki kila mara, lakini linatokana na asili ya mtu huyu mwenyewe.

Mtu yeyote anaweza kutumia maneno na vitendo vyake wenyewe kuwakilisha tabia yake halisi. Sura hii ya kweli bila shaka ni asili yake. Kama wewe ni mtu anayeongea bila kuwa dhahiri, basi una asili mbovu. Kama asili yako ni yenye hila sana, basi namna ambayo unafanya mambo ni janja na laghai sana, nawe unafanya iwe rahisi sana kwa watu kulaghaiwa nawe. Kama asili yako ni mbovu sana, huenda maneno yako ni mazuri kusikiliza, lakini vitendo vyako haviwezi kuficha njia zako mbovu. Kama asili yako ni vivu sana, basi kila kitu unachosema vyote vinalenga kukwepa lawama na wajibu wa uzembe na uvivu wako, na vitendo vyako

vitakuwa vya polepole sana na vizembe, na vizuri sana katika kuuficha ukweli. Kama asili yako ni yenye uwezo wa kuhisi maono ya wengine sana, basi maneno yako yatakuwa yenye busara na hatua zako pia zitalingana sana na ukweli. Kama asili yako ni aminifu sana, basi maneno yako lazima yawe ya dhati na namna ambayo unafanya mambo lazima iwe yenye kuhusika na mambo halisi, bila mengi ya kufanya bwana wako asikuamini. Kama asili yako ni yenye tamaa sana au ni yenye tamaa ya fedha, basi moyo wako mara nyingi utajazwa na mambo haya na utafanya baadhi ya mambo yaliyopotoka bila kukusudia, mambo maovu ambayo hufanya iwe vigumu kwa watu kusahau na zaidi ya hayo yatawaudhi. Kama Nilivyosema, kama una asili ya usaliti basi ni kujinasua kutoka kwake kwa nadra sana. Msiamini kuwa hivyo ndivyo ilivyo kwamba hamna asili ya usaliti kwa sababu hamjamkosea mtu yeyote. Kama hivyo ndivyo unavyofikiri basi unachukiza sana. Maneno ambayo Nimenena kila wakati yamewalenga watu wote, sio tu mtu mmoja au aina ya mtu. Kwa sababu tu hujanisaliti Mimi kwa jambo moja haithibitishi kwamba huwezi kunisaliti katika jambo moja haiashirii kwamba huwezi kunisaliti Mimi katika jambo jingine. Kwa kutafuta ukweli, baadhi ya watu hupoteza imani yao katika kuutafuta ukweli wakati wa kipingamizi katika ndoa zao. Baadhi ya watu huwacha wajibu wao wa kuwa waaminifu Kwangu wakati wa kuvunjika kwa familia. Baadhi ya watu huniacha kwa ajili ya kutafuta wakati wa furaha na msisimko. Baadhi ya watu afadhali waanguke katika korongo lenye giza kuliko kuishi katika mwanga na kupata furaha ya kazi ya Roho Mtakatifu. Baadhi ya watu hupuuza ushauri wa marafiki kwa ajili ya kuridhisha tamaa zao kwa ajili ya mali, na hata sasa hawawezi kuyakubali uovu wao na kugeuza mkondo. Baadhi ya watu wanaishi tu kwa muda chini ya jina Langu ili wapate ulinzi Wangu, wakati wengine hujitolea tu kidogo tu Kwangu kwa kulazimishwa kwa sababu wameyashikilia maisha na wanahofu kifo. Si vitendo hivi na vingine viovu na zaidi ya hayo visivyofaa tabia tu ambazo watu wamenisaliti kwa muda mrefu ndani ya mioyo yao? Bila shaka, Najua usaliti wa watu haukuwa umepangwa mapema, lakini ni ufunuo wa kimaumbile wa asili zao. Hakuna mtu anayetaka kunisaliti, na zaidi ya hayo hakuna mtu aliye na furaha kwa sababu amefanya kitu kunisaliti. Kinyume chake, wanatetemeka kwa hofu, sivyo? Hivyo mnafikiri kuhusu jinsi mnavyoweza kuzikomboa saliti hizi, na jinsi mnavyoweza kubadili hali ya sasa?

Shida Kubwa Sana: Usaliti (2)

Asili ya mwanadamu ni tofauti kabisa na kiini Changu, kwa sababu asili potovu ya mwanadamu hutoka kwa Shetani kabisa; asili ya mwanadamu imetengenezwa na kupotoshwa na Shetani. Yaani, mwanadamu anaishi chini ya ushawishi wa uovu na ubaya wake. Mwanadamu hakui katika ulimwengu wa ukweli au mazingira matakatifu, sembuse mwanadamu kuishi katika nuru. Kwa hiyo, haiwezekani kwa mtu yeyote kuwa na ukweli ndani ya asili yake tangu wakati wa kuzaliwa, sembuse mtu kuweza kuzaliwa na kiini kinachomwogopa na kumtii Mungu.

Badala yake, watu wana asili ambayo humpinga na kumwasi Mungu, na haipendi ukweli. Asili hii ndilo tatizo Ninalotaka kujadili—usaliti. Usaliti ndicho chanzo cha kila mtu kumpinga Mungu. Hili ni tatizo ambalo linapatikana ndani ya mwanadamu tu, na sio ndani Yangu. Wengine watauliza: Kwa kuwa watu wote wanaishi ulimwenguni jinsi tu Kristo aishivyo, mbona watu wote wana asili ambazo zinamsaliti Mungu, ilhali Kristo hana asili hiyo? Hili ni tatizo ambalo lazima muelezwe wazi.

Msingi wa uwepo wa wanadamu ni kuzaliwa upya kwa nafsi tena na tena. Kwa maneno mengine, kila mtu hupata maisha ya kibinadamu katika mwili nafsi yake inapozaliwa upya. Baada ya mwili wa mtu kuzaliwa, maisha yake huendelea hadi mwili unapofikia vikomo vyake hatimaye, ambao ndio wakati wa mwisho, wakati nafsi inapoliacha ganda lake. Utaratibu huu hujirudia tena na tena, nafsi ya mtu ikija na kwenda mara kwa mara, na kwa hiyo uwepo wa wanadamu unadumishwa. Maisha ya mwili pia ni maisha ya nafsi ya mwanadamu, na nafsi ya mwanadamu hukimu uwepo wa mwili wa mwanadamu. Hiyo ni kusema, maisha ya kila mtu hutoka kwenye nafsi yake, na maisha hayana asili katika mwili. Kwa hiyo, asili ya mwanadamu hutoka kwenye nafsi, si kutoka kwa mwili. Nafsi ya kila mtu tu ndiyo inayojua jinsi alivyopitia majaribu, mateso na upotovu wa Shetani. Mwili wa mwanadamu hauyajui mambo haya. Kwa hiyo, bila kujua, wanadamu huwa waovu zaidi, wachafu zaidi, na wabaya zaidi, wakati umbali kati ya mwanadamu na Mimi unazidi kuwa mkubwa, na maisha yanakuwa yenye giza zaidi kwa wanadamu. Shetani huzishika nafsi za wanadamu kwa nguvu, kwa hiyo, bila shaka, mwili wa mwanadamu pia umemilikiwa na Shetani. Mwili kama huo na wanadamu kama hao wangepotea kutompinga Mungu? Wangepotea kulingana naye kiasili? Sababu iliyofanya Nimitupe Shetani chini angani ni kwa sababu alinisaliti. Je, basi wanadamu wanawezaje kutohusishwa? Hii ndiyo sababu usaliti ni asili ya kibinadamu. Ninaamini kwamba mara mnapotea fikira hii, pia mnapaswa kukiamini kiini cha Kristo. Mwili uliovaliwa na Roho wa Mungu ni mwili wa Mungu mwenyewe. Roho wa Mungu ni mwenye mamlaka; Yeye ni mwenye uweza, mtakatifu, na mwenye haki. Vivyo hivyo, mwili Wake pia ni wenye mamlaka, wenye uweza, mtakatifu, na wenye haki. Mwili kama huo unaweza kufanya tu kile ambacho ni cha haki na chenye faida kwa wanadamu, kile ambacho ni kitakatifu, kitukufu na chenye nguvu; Yeye hawezi kutenda jambo lolote ambalo linakiuka ukweli, ambalo linakiuka maadili na haki, sembuse kufanya jambo lolote linaloweza kumsaliti Roho wa Mungu. Roho wa Mungu ni mtakatifu, na kwa hiyo mwili Wake hauwezi kupotoshwa na Shetani; mwili Wake ni wenye kiini tofauti na mwili wa mwanadamu. Kwa maana ni mwanadamu na si Mungu, ambaye anapotoshwa na Shetani; Shetani hawezi kamwe kuupotosha mwili wa Mungu. Kwa hiyo, licha ya ukweli kwamba mwanadamu na Kristo wanaishi katika sehemu sawa, ni mwanadamu tu ndiye anayemilikiwa, anayetumiwa, na anayenaswa na Shetani. Kinyume na hilo, Kristo

hapenyeki kabisa na upotovu wa Shetani, kwa sababu Shetani hatawahi kuweza kupanda hadi mahali pa juu zaidi, na hatawahi kuweza kumkaribia Mungu. Leo, nyote mnapaswa kuelewa kuwa ni wanadamu tu, jinsi walivyopotoshwa na Shetani, ndio hunisaliti. Usaliti hautawahi kuwa suala linalomhusisha Kristo hata kidogo.

Nafsi zote zilizopotoshwa na Shetani zimeshikwa mateka katika miliki ya Shetani. Ni wale tu wanaomwamini Kristo ndio waliotengwa, waliookolewa kutoka katika kambi ya Shetani, na kuletwa ndani ya ufalme wa leo. Watu hawa hawaishi tena chini ya ushawishi wa Shetani. Hata hivyo, asili ya mwanadamu bado imekita mizizi katika mwili wa mwanadamu, yaani, ingawa nafsi zenu zimeokolewa, asili yenu bado ni kama ilivyokuwa awali, na uwezekano kwamba mtanisaliti unabaki kuwa asilimia mia moja. Hii ndiyo sababu kazi Yangu hudumu kwa muda mrefu sana, kwa kuwa asili yenu haiwezi kudhibitiwa kwa urahisi. Sasa, ninyi nyote mnapitia shida kadri ya uwezo wenu mnapotimiza wajibu wenu, ilhali kila mmoja wenu anaweza kunisaliti na kurudi katika miliki ya Shetani, kambini mwake, na kurudia maisha yenu ya zamani—huu ni ukweli usiopingika. Wakati huo, haitawezekana kwenu kudhihirisha chembe ya ubinadamu au mfano wa binadamu, kama mnavyofanya sasa. Katika hali mbaya zaidi, mtaangamizwa, na zaidi ya hayo, mtahukumika milele, mwadhibiwe vikali, msizaliwe upya kamwe. Hii ndiyo shida iliyowekwa mbele yenu. Ninawakumbusha kwa njia hii, kwanza, ili kazi Yangu isiwe imekuwa bure, na pili, ili ninyi nyote mweze kuishi katika siku za nuru. Kwa kweli, kama kazi Yangu ni bure si tatizo la muhimu sana. Kilicho cha muhimu sana ni kwamba mnaweza kuwa na maisha yenye furaha na mustakabali mzuri sana. Kazi Yangu ni kazi ya kuziokoa nafsi za watu. Nafsi yako ikianguka mikononi mwa Shetani, mwili wako hautaishi kwa amani. Ikiwa Ninaulinda mwili wako, hakika nafsi yako pia itakuwa chini ya uangalizi Wangu. Nikikuchukia sana, mwili na nafsi yako vitaanguka mikononi mwa Shetani mara moja. Je, unaweza kukisia hali yako wakati huo? Ikiwa, siku moja mtayapuuza maneno Yangu, basi Nitawakabidhi nyote kwa Shetani, ambaye atawatesa sana hadi hasira Yangu itakapoisha kabisa, au Mimi binafsi Nitawaadhibu ninyi wanadamu wasioweza kuokoleka, kwa kuwa mioyo yenu inayonisaliti haitakuwa imewahi kubadilika.

Nyote mnapaswa sasa kujichunguza haraka iwezekanavyo, ili muone ni kiasi gani cha kunisaliti kimebaki ndani yenu. Ninangojea jibu lenu kwa pupa. Msiwe wazembe katika kunishughulikia. Kamwe Mimi huwa sichezi michezo na watu. Nikisema Nitatenda jambo basi hakika Nitalitenda. Natumai kila mmoja wenu atakuwa mtu anayeyachukulia maneno Yangu kwa uzito, na asifikirie kana kwamba maneno hayo ni ubuni wa sayansi. Ninachotaka ni kitendo thabiti kutoka kwenu, siyo mawazo yenu. Baadaye, lazima mjibu maswali Yangu, ambayo ni kama ifuatavyo: 1. Ikiwa kwa kweli wewe ni mtendaji huduma, je, unaweza kutoa huduma Kwangu kwa uaminifu, bila dalili yoyote ya uzembe au mtazamo hasi? 2. Je, ukigundua kuwa

Sijawahi kukuthamini, bado utaweza kusalia na kunitolea huduma ya maisha yote? 3. Ikiwa bado Ninakudharau sana licha ya wewe kutumia bidii nyingi, je, utaweza kuendelea kunifanyia kazi katika mashaka? 4. Ikiwa, baada ya wewe kufanya matumizi kwa ajili Yangu, Siyaridhishi mahitaji yako madogo, je, utavunjika moyo na kusikitishwa na Mimi, au hata ukasirike na kunitukana kwa sauti kubwa? 5. Ikiwa daima umekuwa mwaminifu sana, ukinipenda sana, ilhali unateseka na ugonjwa, umaskini, na kutengwa na marafiki na jamaa zako, au ikiwa unavumilia taabu nyingine zozote maishani, bado uaminifu na upendo wako Kwangu utaendelea? 6. Ikiwa hakuna lolote kati ya yale ambayo umefikiria moyoni mwako linalingana na kile ambacho Nimefanya, je, utaitembea njia yako ya baadaye kwa namna gani? 7. Ikiwa hupokei lolote kati ya mambo ambayo ulitarajia kupokea, je, unaweza kuendelea kuwa mfuasi Wangu? 8. Ikiwa hujawahi kuelewa kusudi na umuhimu wa kazi Yangu, je, unaweza kuwa mtu mtiifu ambaye hatoi hukumu kiholela na kufanya maamuzi? 9. Je, unaweza kuthamini maneno yote ambayo Nimeyanena na kazi yote ambayo Nimeifanya wakati Nimekuwa pamoja na wanadamu? 10. Je, unaweza kuwa mfuasi Wangu mwaminifu, aliye tayari kuvumilia mateso ya maisha kwa ajili Yangu, ingawa hupokei chochote? 11. Je, unaweza kuachilia kuzingatia, kupanga, au kuandaa njia yako ya kuendelea kuishi ya siku za baadaye kwa ajili Yangu? Maswali haya yanawakilisha mahitaji Yangu ya mwisho ninayotaka kutoka kwenu, nami Natumai kuwa ninyi nyote mnaweza kunipa majibu. Ikiwa umetimiza jambo moja au mawili ambayo maswali haya yanataka ufanye, basi lazima uendelee kujitahidi. Ikiwa huwezi kutimiza hata moja kati ya mahitaji haya, hakika wewe ni aina ya mtu ambaye atatupwa kuzimu. Sihitaji kusema chochote zaidi kwa watu kama hawa, kwa sababu hakika wao sio watu ambao wanaweza kukubaliana nami. Je, Ninawezaje kumweka nyumbani Kwangu mtu ambaye anaweza kunisaliti katika hali yoyote ile? Kwa wale ambao bado wanaweza kunisaliti katika hali nyingi, Nitazingatia utendaji wao kabla ya kufanya mipango mingine. Hata hivyo, wote wanaoweza kunisaliti, bila kujali ni chini ya hali gani, Sitawahi kusahau; Nitawakumbuka moyoni Mwangu, na kungojea fursa ya kulipiza matendo yao maovu. Mahitaji yote ambayo Nimeibua ni shida ambazo lazima nyote mzichunguze ndani yenu wenyewe. Natumai ninyi nyote mnaweza kuyazingatia kwa makini na kutonishughulika kwa uzembe. Hivi karibuni, Nitaangalia majibu ambayo mmenipa dhidi ya mahitaji Yangu. Kufikia wakati huo, Sitahitaji chochote zaidi kutoka kwenu na Sitawapa onyo lenye ari zaidi. Badala yake, Nitatumia mamlaka Yangu. Wale wanaopaswa kuhifadhiwa watahifadhiwa, wale wanaopaswa kupewa thawabu watapewa thawabu, wale wanaopaswa kukabidhiwa kwa Shetani watakabidhiwa kwa Shetani, wale wanaopaswa kuadhibiwa vikali wataadhibiwa vikali, na wale wanaopaswa kuangamia wataangamizwa. Kwa hiyo, hakutakuwa tena na mtu wa kunisumbua katika siku Zangu. Je, unaamini maneno Yangu? Je, unaamini kulipiza kisasi? Je, unaamini kuwa Nitawaadhibu wale waovu wote wanaonidanganya na kunisaliti? Je, unatarajia siku hiyo ije haraka au ije baadaye? Je, wewe ni mtu ambaye anaogopa adhabu, ama mtu ambaye angenipinga

ingawa lazima avumilie adhabu? Siku hiyo itakapowadia, unaweza kukisia ikiwa utaishi katikati ya shangwe na kicheko, au ikiwa utalia na kusaga meno yako? Je, unatarajia kukumbana na mwisho wa aina gani? Je, umewahi kufikiria kwa uzito ikiwa unaniamini asilimia mia moja au una tashwishi nami asilimia mia moja? Je, umewahi kufikiria kwa uangalifu matendo na mwenendo wako vitakuletea matokeo ya aina gani? Je, unatumaini kwa kweli kuwa maneno Yangu yote yatatimizwa, ama unaogopa kuwa maneno Yangu yatatimizwa kama matokeo? Ikiwa unatumaini kuwa Nitaondoka hivi karibuni ili Niyatimize maneno Yangu, je, unapaswa kuyachukuliaje maneno na matendo yako mwenyewe? Ikiwa hutumainii kuondoka Kwangu na hutumaini maneno Yangu yote yatimizwe mara moja, kwa nini uniamini hata kidogo? Kwa kweli unajua mbona unanifuata? Ikiwa sababu yako ni kupanua upeo wako tu, hakuna haja ya kujisumbua kufanya hivyo. Ikiwa ni ili ubarikiwe na kuepukana na msiba unaokuja, mbona hujali kuhusu tabia yako mwenyewe? Mbona hujiulizi ikiwa unaweza kuyakidhi mahitaji Yangu? Mbona pia hujiulizi ikiwa unastahili kupokea baraka zitakazokuja?

Amri Kumi za Utawala Ambazo Lazima Wateule wa Mungu katika Enzi ya Ufalme Wazitii

1. Mwanadamu hapaswi kujitukuza wala kujipa sifa. Anapaswa kumwabudu na kumsifu Mungu.

2. Unapaswa kufanya lolote ambalo lina manufaa kwa kazi ya Mungu, na hupaswi kufanya chochote ambacho kitaleta madhara kwa manufaa ya kazi ya Mungu. Unapaswa kutetea jina la Mungu, ushahidi Wake, na kazi ya Mungu.

3. Pesa, vitu vya dunia, na mali yote ambayo yako katika kaya ya Mungu ni sadaka ambazo zinapasa kutolewa na binadamu. Sadaka hizi hazifai kufurahiwa na binadamu yeyote ila kasisi na Mungu Mwenyewe, kwani sadaka zinazotolewa na binadamu ni za kufurahiwa na Mungu, Mungu pekee ndiye Anayeweza kumgawia kasisi sadaka hizi, na hakuna mwingine yeyote aliyehitimu wala kuwa na haki ya kufurahia sehemu yoyote ya sadaka hizi. Sadaka zote zinazotolewa na mwanadamu (ikiwemo pesa na vitu vinavyoweza kufurahiwa) vinapewa Mungu, na sio kwa mwanadamu. Na hivyo, vitu hivi havipaswi kufurahiwa na mwanadamu; iwapo mwanadamu angevifurahia vitu hivi, basi angekuwa anaiba sadaka. Yeyote yule atakayefanya hili ni msaliti kama Yuda, kwa kuwa, zaidi ya Yuda kuwa msaliti. Yuda alijitwalia vilivyokuwa katika mfuko wa hela.

4. Mwanadamu anayo tabia ya upotovu na, zaidi ya hayo, amejawa na hisia. Kwa hivyo, ni marufuku kabisa kwa watu wa jinsia mbili tofauti kufanya pamoja kazi wakati wa kumtumikia Mungu bila kuwepo na mtu mwingine. Yeyote yule atakayepatikana na kosa hili atatupiliwa

mbali, bila ubaguzi—na hakuna atakayeepuka hili.

5. Hupaswi kumhukumu Mungu, au kujadili kwa kawaida mambo yanayomuhusu Mungu. Unapaswa kutenda vile mwanadamu anavyopaswa kutenda, na kuzungumza jinsi mwanadamu anapasa kuzungumza, na hupaswi kuvuka upeo wako wala kuvuka mipaka yako. Uchungu ulimi wako na uwe mwangalifu na hatua zako. Yote haya yatakuzuia kufanya jambo lolote linaloweza kukosea tabia ya Mungu.

6. Unapaswa kufanya yale yanayopaswa kufanywa na mwanadamu, na kutenda wajibu wako, na kutimiza majukumu yako, na kushikilia jukumu lako. Kwa sababu unaamini katika Mungu, unapasa kutoa mchango wako kwa kazi ya Mungu; kama huwezi, basi wewe hufai kula na kunywa maneno ya Mungu, na hufai kuishi katika nyumba ya Mungu.

7. Katika kazi na mambo yanayohusiana na kanisa, kando na kumtii Mungu, katika kila kitu unapaswa kufuata maagizo ya mwanadamu anayetumiwa na Roho Mtakatifu. Hata kosa lolote hata liwe dogo kivipi halikubaliwi. Lazima uwe mkamilifu katika kutii kwako, na hupaswi kuchunguza kati ya mazuri na mabaya; yaliyo mazuri au mabaya hayakuhusu. Unapaswa kujishughulisha tu na utiifu kamili.

8. Watu wanaoamini katika Mungu wanapaswa kumtii na kumwabudu. Hupaswi kusifu au kumwabudu mtu yeyote; hupaswi kumpa Mungu nafasi ya kwanza, binadamu unayemheshimu nafasi ya pili, kisha wewe mwenyewe nafasi ya tatu. Mtu yeyote asishikilie nafasi yoyote moyoni mwako, na hufai kuzingatia watu—hasa wale unaowaenzi—kuwa katika kiwango sawa na Mungu, kuwa sawa na Yeye. Mungu hawezi kustahimili hili.

9. Mawazo yako yanapasa kuwa ya kazi ya kanisa. Unapaswa kuweka kando matarajio ya mwili wako, uwe na msimamo thabiti kuhusu mambo ya kifamilia, na ujitoe kwa moyo wako wote kwa kazi ya Mungu, na uiweke kazi ya Mungu kwanza kisha maisha yako katika nafasi ya pili. Huu ndio mwenendo mwema wa utakatifu.

10. Jamaa zako (watoto, mke au mume, dada zako au wazazi wako na kadhalika) wasio wa imani yako hawapaswi kulazimishwa kuja kanisani. Nyumba ya Mungu haina ukosefu wa washirika, na hakuna haja ya kuijaza na watu wasiokuwa na maana katika nyumba Yake. Wale wote wasioamini kwa moyo mchangamfu, hawapaswi kuongozwa kuingia kanisani. Amri hii inaelekezwa kwa kila mwanadamu. Kuhusu hili jambo mnapaswa kuchunguza, mfuatilie na mkumbushane, na hakuna anayepasa kukiuka amri hii. Hata jamaa wako wasio wa imani yako wanapoingia kanisani shingo upande, hawapaswi kupatiwa jina jipya wala kupewa vitabu vya kanisa; watu kama hao si wa kaya ya Mungu, na kuingia kwao kanisani kunapaswa kukomeshwa kwa udi na uvumba. Iwapo matatizo yataletwa kanisani kwa sababu ya uvamizi wa mapepo, basi

wewe mwenyewe utafukuzwa au kuwekewa vikwazo. Kwa ufupi, kila mmoja analo jukumu katika hili jambo, lakini pia hupasi kuwa asiyejali, wala kutumia jambo hili kulipiza kisasi cha kibinafsi.

Mnapaswa Kuzingatia Matendo Yenu

Kulingana na vitendo na matendo katika maisha yenu, nyote mnahitaji kurasa za maneno ya kuwajaza na kuwajenga kila siku, kwani mko na upungufu mno, na ujuzi na maarifa yenu ya kupokea ni ya hali ya chini sana. Katika maisha yenu ya kila siku, mnaishi katika hali na mazingira yasiyo na ukweli ama fahamu nzuri. Hamna rasilimali ya uwepo na pia hamna msingi wa Kunijua au kujua ukweli. Imani yenu imejengwa tu juu ya ujasiri usio dhahiri au kwenye ibada za kidini na ujuzi kulingana na mafundisho ya kidini kabisa. Kila siku Ninatazama mienendo yenu na kuchunguza nia yenu na matunda yenu maovu. Sijawahi kumpata mmoja ambaye kwa kweli aliweka moyo wake na roho yake kwenye madhabahu Yangu, ambayo hayajawahi kusonga. Kwa hivyo, Singependa kuyamwaga bure maneno yote ambayo Nina nia ya kumwelezea mwanadamu wa aina hii. Moyoni Mwangu, Ninapanga kuikamilisha kazi Yangu iliyosalia tu na kuleta wokovu kwa mwanadamu ambaye Sijamwoko bado. Hata hivyo, Ningependa wale wote wanaonifuata wapokee wokovu Wangu na ukweli ambao neno Langu linaweka katika mwanadamu. Natumaini kuwa siku moja unapofumba macho yako, utauona ulimwengu ambamo manukato yametanda hewani na vijito vya maji ya uhai vinatiririka, na wala siyo dunia baridi isiyoonekana vizuri ambapo mawingu meusi hutia anga doa na ambamo vilio vya kughadhabisha havikomi.

Kila siku, fikira na matendo ya kila mmoja yanachunguzwa na Yeye na, katika wakati uo huo, wamo katika matayarisho ya siku zao zinazofuata. Hii ni njia ambayo lazima kila mtu aliye hai aipitie na ambayo Nimeamulia kabla kila mmoja. Hakuna anayeweza kuepuka hili na hakuna atakayepata upendeleo. Nimezungumza maneno yasiyohesabika na zaidi ya yote Nimefanya kazi kubwa mno. Kila siku, Ninatazama vile kila mwanadamu kiasili anafanya yote ambayo anafaa kufanya kulingana na asili yake na vile inavyoendelea. Bila kujua, wengi tayari wamo katika “njia sahihi”, ambayo Niliweka kwa ufunuo wa mwanadamu wa kila aina. Tayari Nimemweka kila aina ya mwanadamu katika mazingira tofauti tofauti, na katika sehemu zao, kila mmoja amekuwa akionyesha tabia zake za asili. Hakuna mtu wa kuwafunga, hakuna mtu wa kuwatongoza. Wako huru katika nafsi yao yote na lile wanalolieleza linakuja kwa wepesi. Kuna kitu kimoja tu ambacho huwaweka katika nidhamu, na hayo ni maneno Yangu. Kwa hivyo watu wengine huyasoma maneno Yangu shingo upande, bila kuyatenda kamwe, wakifanya hivyo ili kuepuka kifo tu. Kwa upande mwingine, wanadamu wengine huona ugumu kuvumilia siku bila maneno Yangu kuwaelekeza na kuwapa, kwa hivyo wao hushikilia maneno Yangu kiasili wakati

wote. Muda unavyopita, wao basi hugundua siri ya maisha ya mwanadamu, hatima ya mwanadamu na thamani ya kuwa na utu. Mwanadamu si zaidi ya haya katika uwepo wa maneno Yangu, na Mimi huruhusu tu mambo yachukue mkondo wake. Sifanyi chochote kinachomlazimisha mwanadamu kuishi kulingana na maneno Yangu kama msingi wa kuwepo kwake. Na kwa hivyo wale wasiokuwa na dhamiri au thamani katika kuwepo kwao hutazama kwa kimya mambo yanavyoenda kisha wanayatupa maneno Yangu kando kwa ujasiri na kufanya vile wanavyopenda. Wanaanza kuchoshwa na ukweli na mambo yote yatokayo Kwangu. Isitoshe, wao huchoka kukaa katika nyumba Yangu. Wanadamu hawa hukaa katika nyumba Yangu kwa ufupi tu kwa ajili ya hatima zao na kuepuka adhabu, hata kama wanafanya huduma. Lakini nia zao huwa hazibadiliki, wala matendo yao. Hii huendeleza zaidi hamu zao za Baraka, hamu za njia moja kwenda katika ufalme ambako wanaweza kubakia milele, na pia njia ya kuingia mbingu ya milele. Jinsi wanavyotamani zaidi siku Yangu ije hivi karibuni, ndivyo wanavyohisi zaidi kuwa ukweli umekuwa kizingiti, kizuizi njiani mwao. Wanangoja kwa hamu kuingia katika ufalme ili wafurahie daima baraka za ufalme wa mbinguni, bila kutaka kuufuata ukweli ama kukubali hukumu na kuadibu, na zaidi ya yote, bila kuhitaji kuishi kwa utumishi katika nyumba Yangu na kufanya vile Ninavyoamuru. Wanadamu hawa hawaingii katika nyumba Yangu kuukamilisha moyo unaotaka kujua ukweli wala kufanya kazi pamoja na uongozi Wangu. Lengo lao tu ni wawe miongoni mwa wale ambao hawataangamizwa katika enzi inayofuata. Kwa hivyo nyoyo zao hazijawahi kuujua ukweli wala kujua jinsi ya kuukubali ukweli. Hii ndiyo sababu wanadamu wa aina hii hawajawahi kutia vitendoni ukweli au kujua undani wa ufisadi wao, ilhali wameishi katika nyumba yangu kama “wajakazi” mpaka mwisho. Wanangoja “kwa uvumilivu” kuja kwa siku Yangu, na hawachoki wanaporushwa huku na kule na hali ya kazi Yangu. Haijalishi bidii zao ni kubwa namna gani au ni gharama gani wamelipa, hakuna atakayeona kuwa wameteseka kwa ajili ya ukweli ama kujitoa kwa ajili Yangu. Katika mioyo yao, wanangoja kwa hamu siku ambayo Nitakomesha enzi nzee, na zaidi ya hayo, wanangoja kwa hamu kujua jinsi nguvu na mamlaka Yangu ni kuu. Kile hawajawahi kimbilia kufanya ni kujibadilisha na kufuata ukweli. Wanapenda kile kinachonichosha na kuchoshwa na kile ninachopenda. Wanangoja kwa hamu kile Ninachokuwa na kinyongo nacho lakini wakati uo huo wanaogopa kupoteza kile Ninachochukia. Wanaishi katika dunia hii yenye maovu ila hawajawahi kuwa na chuki nayo na wana hofu sana kuwa Nitaangamiza dunia hii. Nia walizo nazo zinakanganya: Wanapendezwa na dunia hii Ninayochukia, na kwa wakati uo huo wanangoja kwa hamu Niiharibu dunia hii hivi karibuni. Kwa njia hii, wataepuka mateso ya uharibifu na wabadilishwe kuwa watawala wa enzi mpya kabla hawajapotoshwa kutoka katika njia ya kweli. Hii ni kwa sababu hawapendi ukweli na wanahofia kila kitu kitokacho Kwangu. Huenda ikawa watakuwa “watu watiifu” kwa muda mfupi kwa minajili ya kutopoteza baraka, lakini fikira zao za kungoja baraka kwa hamu na woga wao wa kuangamia na kuingia katika

ziwa la moto haziwezi kulingwa kuonekana. Siku Yangu inapokaribia, hamu zao zinazidi kuimarika. Na vile janga lilivyo kubwa, ndivyo wanavyopoteza tumaini wasijue watakapoanzia ili kunifanya Nifurahi na kuzuia wasipoteze baraka ambazo wamezingoja kwa muda mrefu. Pindi mkono Wangu unapoanza kazi yake, wanadamu hawa wana hamu kuchukua hatua kuhudumu kama watangulizi. Wanafikiri tu kusonga kwa nguvu mpaka mstari wa mbele wa majeshi, wakiwa na woga mwingi kuwa Sitawaona. Wanafanya na kusema kile wanachodhani ni ukweli, bila kujua kuwa vitendo na matendo yao hayajawahi na umuhimu kwa ukweli, na kuwa hutatiza na kuingilia tu mipango Yangu. Hata ingawa wanaweza kuwa wameweka juhudi nyingi na wanaweza kuwa wa kweli katika ridhaa na nia zao kustahimili ugumu, kila wanachokifanya hakihusiani na Mimi, kwa maana Sijaona hata mara moja kwamba matendo yao yametoka kwa nia njema, na zaidi ya hayo, Sijawaona kama wameweka kitu chochote kwenye madhabahu Yangu. Hayo ndiyo matendo yao mbele Yangu kwa miaka hii mingi.

Mwanzoni, Nilitaka kuwapa ukweli zaidi, lakini kwa sababu mtazamo wenu kwa ukweli ni baridi sana na usiojali, Nimesalimu amri. Sipendi kuona jitihada Zangu zikipotea bure, na pia Sipendi kuwaona watu wakishika maneno Yangu na ilhali katika kila kipengele wakifanya yale ya Kunipinga Mimi, kunidhuru Mimi, na kunikufuru. Kwa sababu ya mtazamo wenu na utu wenu, Ninawapa sehemu kidogo tu ya maneno yaliyo muhimu zaidi kwenu kama jaribio Langu kwa wanadamu. Ni mpaka sasa ndiyo Naweza thibitisha kwa hakika kwamba uamuzi na mipango Niliyoweka ni kulingana na yale mnayohitaji na kuwa mtazamo Wangu kwa wanadamu uko sawa. Miaka yenu mingi ya matendo mbele Yangu imenipa jibu ambalo Sijawahi kupata hapo awali. Na swali la jibu hili ni: “Mtazamo wa mwanadamu mbele ya ukweli na Mungu wa ukweli ni upi?” Juhudi ambazo Nimemwagia mwanadamu ni dhihirisho la kiini Changu cha kumpenda mwandamu, na vitendo na matendo ya mwanadamu mbele Yangu pia yamedhihirisha kiini cha mwanadamu cha kuchukua ukweli na kunipinga Mimi. Katika wakati wote Mimi hujali wale wote ambao wamenifuata, lakini hakuna wakati ambao wale wanaonifuata wameweza kupokea neno Langu; hawana uwezo kabisa wa kukubali hata maoni yanayotoka Kwangu. Hili ndilo hunihuzunisha zaidi ya yote. Hakuna anayeweza kunielewa na, zaidi ya hayo, hakuna anayeweza kunikubali, hata ingawa mtazamo Wangu ni wa kweli na maneno Yangu ni ya upole. Wote wanafanya kazi Niliyowaaminia kuifanya kulingana na fikira zao; hawatafuti nia Zangu, wala kuuliza maombi Yangu. Bado wanadai kuwa Wananihudumia kwa uaminifu, wakati huu wote wakiwa wananiasi. Wengi wanaamini kuwa ukweli usiokubalika nao au ukweli ambao hawawezi kutia vitendoni sio ukweli. Kwa watu kama hawa, ukweli Wangu unakuwa kitu cha kukataliwa na kutupiliwa kando. Kwa wakati uo huo Ninakuwa mmoja anayetambuliwa na mwanadamu kwa neno tu kama Mungu, lakini pia kuchukuliwa kama mtu wa nje ambaye sio ukweli, njia na uhai. Hakuna anyejua ukweli huu: Maneno yangu ndio ukweli usiobadilika

milele. Mimi Ndiye msambazaji wa binadamu na kiongozi wa pekee wa mwanadamu. Thamani na maana ya maneno Yangu haibainishwi na kama yanakubaliwa au kutambuliwa na mwanadamu, ila ni kwa kiini cha maneno yenyewe. Hata kama hakuna mtu hata mmoja duniani anaweza kupokea maneno Yangu, thamani ya maneno Yangu na usaidizi wake kwa mwanadamu hayapimiki na mwanadamu yeyote. Kwa hivyo, Ninapokumbwa na wanadamu wengi wanaoasi, kukataa au kudharau kabisa maneno Yangu, msimamo Wangu ni huu tu: Wacha wakati na ukweli uwe shahidi Wangu na uonyeshe kuwa maneno Yangu ndiyo ukweli, njia na uhai. Wacha vionyeshe kuwa yote Niliyosema ni ya ukweli, na kuwa ni yale ambayo mwanadamu lazima apewe, na, zaidi ya yote, yale ambayo mwanadamu anafaa akubali. Nitawaruhusu wote wanaonifuata wajue ukweli huu: Wote wasioyakubali maneno Yangu kikamilifu, wale wasiyoaweka maneno Yangu katika vitendo, wale wasiopata sababu ndani ya maneno Yangu, na wale wasiopata wokovu kwa sababu ya maneno Yangu, ni wale ambao wamehukumiwa na maneno Yangu na, zaidi ya hayo, wamepoteza wokovu Wangu, na fimbo Yangu haitaondoka kamwe miongoni mwao.

Aprili 16, 2003

Mungu Ndiye Chanzo cha Uhai wa Mwanadamu

Tangu unapoingia katika dunia hii ukilia, unaanza kutekeleza wajibu wako. Kwa kuchukua jukumu lako katika mpango wa Mungu na katika utaratibu Wake, unaanza safari yako katika maisha. Licha ya asili yako na licha ya safari iliyoko mbele yako, hakuna kitakachoeputa mpango na utaratibu ambao mbingu imeunda, na hakuna aliye na udhibiti wa hatima yake mwenyewe, kwa maana yule Anayetawala kila kitu ndiye tu Aliye na uwezo wa kazi hiyo. Tangu siku aliyoumbwa binadamu, Mungu amekuwa akitenda kazi Yake kwa njia hii, kusimamia ulimwengu huu na kuelekeza mifuatano ya mabadiliko katika mambo yote na njia ambazo yanasongea. Pamoja na vitu vyote vingine, mwanadamu polepole na bila kujua anastawishwa na utamu na mvua na umande kutoka kwa Mungu. Kama vitu vyote vingine, mwanadamu bila kujua, anaishi chini ya mpango wa mkono wa Mungu. Moyo na roho ya mwanadamu vimeshikwa katika mkono wa Mungu, na maisha yake yote yanatazamwa machoni mwa Mungu. Haijalishi kama unayaamini mambo haya au la, vitu vyote, viwe hai au vilivyokufa, vitahamishwa, vitabadilika, kufanywa vipya, na kutoweka kulingana na mawazo ya Mungu. Hii ndiyo njia ambayo Mungu huongoza vitu vyote.

Usiku uingiaipo polepole, mwanadamu huwa hafahamu, kwani moyo wa mwanadamu hauwezi kujua jinsi giza linapokaribia au wapi linakotoka. Usiku unapotoweka polepole, mwanadamu hukaribisha mwanga wa mchana, lakini ikija kwa kulikotoka nuru na jinsi

imeliondoa giza la usiku, mwanadamu anajua hata machache na hata ana ufahamu mchache zaidi Mabadiliko haya ya kawaida ya mchana na usiku humpitisha mwanadamu kutoka kipindi kimoja hadi kingine, kutoka kipindi kimoja cha kihistoria hadi kingine, wakati huu wote yakihakikisha kwamba kazi ya Mungu katika kila kipindi na mpango Wake wa kila enzi unatekelezwa. Mwanadamu ametembea katika enzi hizi tofauti pamoja na Mungu, lakini bado hafahamu kwamba Mungu huongoza hatima ya mambo yote na viumbe hai au jinsi Mungu hupanga na kuelekeza mambo yote. Hili ni jambo ambalo limekwepa ufahamu wa binadamu tangu enzi za kale mpaka leo. Kuhusu sababu, siyo kwa sababu matendo ya Mungu hayafahamiki, au kwa sababu mpango wa Mungu bado haujakamilika, lakini ni kwa sababu moyo na roho ya mwanadamu viko mbali sana na Mungu, kiasi ya kwamba, mwanadamu anabaki katika huduma ya Shetani wakati ule ule anapomfuata Mungu—na hata halitambui hili. Hakuna anayetafuta nyayo za Mungu kwa vitendo au kuonekana Anakoonyesha, na hakuna aliye na hiari ya kuwepo katika huduma na utunzaji wa Mungu. Badala yake, wao wako tayari kutegemea upotoshaji wa Shetani, yule mwovu, ili kurekebisha kufuatana na dunia hii na kanuni za kuwepo ambazo watu waovu hufuata. Wakati huu, moyo na roho za mwanadamu hutolewa ushuru kwa shetani na kuwa riziki ya Shetani. Hata zaidi, moyo wa binadamu na roho yake zimekuwa mahali ambapo Shetani anaweza kuishi na uwanja wake wa kuchezea unaofaa. Kwa njia hii, mwanadamu kwa kutojua hupoteza ufahamu wake wa kanuni za kuwa binadamu, na wa thamani na maana ya kuwepo kwa binadamu. Sheria za Mungu na agano kati ya Mungu na mwanadamu huangamia hatua kwa hatua kutoka katika moyo wa mwanadamu, na yeye huacha kumtafuta na kumsikiza Mungu. Wakati upitavyo, mwanadamu haelewi tena kwa nini Mungu alimuumba, wala haelewi maneno yanayotoka katika kinywa cha Mungu na yote yanayotoka kwa Mungu. Mwanadamu kisha huanza kupinga sheria na amri za Mungu na moyo na roho zake hufishwa.... Mungu humpoteza mwanadamu ambaye Alimuumba mwanzoni, na mwanadamu hupoteza mzizi wa mwanzo wake: Hii ndiyo huzuni ya hii jamii ya wanadamu. Kusema ukweli, tangu mwanzo mpaka sasa, Mungu amepanga janga kwa wanadamu, ambapo mwanadamu ni mhusika mkuu na mwathiriwa; kuhusu nani ndiye mwelekezi wa hadithi hii ya janga, hakuna anayeweza kujibu.

Katika upana mkubwa wa dunia hii, mabadiliko yasiyohesabika yamefanyika, bahari kujaa hadi kuziba mashamba, mashamba kufurika hadi baharini, tena na tena. Isipokuwa Yule ambaye anatawala kila kitu katika ulimwengu, Hakuna anayeweza kuongoza na kuelekeza jamii hii ya wanadamu. Hakuna yeyote hodari kufanya kazi au kufanya maandalizi kwa ajili ya jamii hii ya binadamu, sembuse yule anayeweza kuongoza jamii hii ya wanadamu hadi hatima ya mwanga na kuikomboa kutokana na udhalimu wa duniani. Mungu hulalamikia wakati ujao wa wanadamu, huhuzunishwa na kuanguka kwa mwanadamu na anaumizwa kwamba binadamu wanatembea, hatua baada ya nyingine hadi kuoza na katika njia ambayo hawawezi kurudi. Wanadamu ambao

wameuvunja moyo wa Mungu na wakamkana kumfuata yule mwovu: je, kuna yeyote ambaye amewahi kuwaza kuhusu mwelekeo ambao wanadamu wa aina hii huenda wanafuata? Ni kwa sababu hii haswa kwamba hakuna anayehisi hasira ya Mungu, hakuna anayetafuta njia ya kumpendeza Mungu au kujaribu kuja karibu na Mungu na isitoshe, hakuna anayetafuta kufahamu huzuni na maumivu ya Mungu. Hata baada ya kusikia sauti ya Mungu, binadamu anaendelea tu kwenye njia yake mwenyewe, anazidi kwenda mbali na Mungu, kukwepa neema na huduma ya Mungu, na kuepuka ukweli Wake, akiona heri kujiuza kwa Shetani, adui wa Mungu. Na ni nani amefikiri—iwapo mwanadamu ataendelea kuwa mkaidi—jinsi Mungu atakavyowatendea wanadamu hawa ambao wamempuuza bila kusita? Hakuna anayejua kwamba maana ya ukumbusho wa mara kwa mara na kusihi kwa Mungu ni kwa sababu Yeye anayo katika mikono yake maafa yasiyokuwa ya kawaida ambayo ameandaa, maafa ambayo yatakuwa magumu kwa mwili na nafsi ya mwanadamu kustahimili. Maafa haya siyo tu adhabu ya mwili bali pia ya roho. Unafaa kujua hili: Mpango wa Mungu utakaposhindikana na wakati makumbusho Yake na kusihi Kwake hakutapata majibu yoyote, atatoa hasira ya aina gani? Hii itakuwa kama kitu ambacho hakijawahi kushuhudiwa hapo awali au hata kusikika na viumbe vyovyote. Na hivyo Nasema, majanga haya hayana mengine ya kulinganishwa nalo awali na kamwe hayatawahi kurudiwa. Hii ni kwa sababu ni mpango wa Mungu kuumba wanadamu mara hii moja tu na kuwaokoa wanadamu mara hii moja tu. Hii ndiyo mara ya kwanza na pia ni ya mwisho. Kwa hivyo, hakuna anayeweza kuelewa nia za bidii na hamu ya ari ambazo kwazo Mungu huokoa wanadamu wakati huu.

Mungu aliumba dunia hii na kuleta mwanadamu, kiumbe hai ambaye alitia uhai ndani yake. Kisha, mwanadamu akaja kuwa na wazazi na jamaa na hakuwa mpweke tena. Tangu mwanadamu alipotua macho kwa mara ya kwanza katika dunia hii ya mali, ilibainika kuwa angeishi ndani ya utaratibu wa Mungu. Ni pumzi ya uhai kutoka kwa Mungu ndiyo hustawisha kila kiumbe hai katika ukuaji wake hadi kinapokomaa. Wakati wa mchakato huu, hakuna anayehisi kwamba mwanadamu anakua chini ya uangalizi wa Mungu, bali badala yake anaamini kwamba mwanadamu anafanya hivyo chini ya utunzaji wa upendo wa wazazi wake, na kwamba ni silika yake mwenyewe ya maisha ambayo inaongoza mchakato huu wa kukua kwake. Hii ni kwa sababu mwanadamu hajui aliyeleta maisha au yalikotoka maisha hayo, sembuse jinsi silika ya maisha husababisha miujiza. Anajua tu kwamba chakula ndicho msingi wa kuendelea kwa maisha yake, kwamba uvumilivu ndio chanzo cha kuwepo kwake, na kwamba imani zilizomo akilini mwake ndizo raslimali ambazo kwazo kuendelea kuishi kwake kunategemea. Mwanadamu hajui kabisa kuhusu neema na riziki zitokazo kwa Mungu, na kwa njia hii yeye hupoteza. uzima aliopewa na Mungu bila azma.... Hakuna hata mmoja wa wanadamu hawa ambaye Mungu anamwangazia usiku na mchana huchukua jukumu la kumwabudu. Mungu

anaendelea tu kufanya kazi juu ya mwanadamu, akiwa hana matarajio yoyote kutoka kwake, kama jinsi ambavyo Amepanga. Anafanya hivyo kwa matumaini kwamba siku moja, mwanadamu ataamka kutoka katika ndoto yake na ghafla kuelewa thamani na maana ya maisha, gharama aliyolipa Mungu kwa yote ambayo Amempa, na wasiwasi wa hamu ambao kwao Mungu anangoja mwanadamu amgeukie. Hakuna yeyote amewahi kuchunguza siri zinazoongoza asili na kuendelea kwa maisha ya mwanadamu. Ni Mungu tu, ambaye Anaelewa yote haya, kwa kimya huvumilia mapigo na maumivu ambayo binadamu, ambaye amepokea kila kitu kutoka kwa Mungu lakini bila shukurani, humpa. Binadamu huchukulia kila kitu kinacholetwa na maisha kimzaha, na, vilevile, nini “jambo lisilo na shaka,” kwamba Mungu anasalitiwa na mwanadamu, anasahaulika na mwanadamu, na kutozwa kwa nguvu na mwanadamu. Je, inaweza kuwa kwamba mpango wa Mungu ni wa maana namna hii kweli? Je inaweza kuwa kwamba mwanadamu, kiumbe huyu hai ambaye alitoka katika mkono wa Mungu, ni wa maana namna hiyo kweli? Mpango wa Mungu hakika ni wa umuhimu kabisa; hata hivyo, kiumbe chenye uhai kilichoumbwa na mkono wa Mungu kipo kwa ajili ya mpango Wake. Kwa hivyo, Mungu hawezi kuuharibu mpango Wake kwa sababu ya chuki kwa jamii hii ya wanadamu. Ni kwa ajili ya mpango Wake na kwa ajili ya pumzi aliyotoa ndiyo maana Mungu hustahimili mateso yote, sio kwa ajili ya mwili wa mwanadamu ila ni kwa sababu ya uhai wa mwanadamu. Yeye hufanya hivyo ili kurudisha pumzi Aliyopuliza ndani mwa mwanadamu, wala sio nyama za mwili. Huu ndio mpango wake.

Wote wanaokuja duniani humu lazima wapitie maisha na kifo, na wengi wao walipitia mzunguko wa kifo na kuzaliwa upya. Wale wanaoishi watakufa hivi karibuni na wafu watarejea karibuni. Yote haya ni mwendo wa maisha uliopangwa na Mungu kwa kila kiumbe hai. Hata hivyo, njia hii na mzunguko huu hasa ni ukweli ambao Mungu anataka binadamu aone: kwamba uzima aliopewa mwanadamu na Mungu hauna mipaka, na hauzuiliwi na maumbile ya nje, wakati, au nafasi. Hili ndilo fumbo la uzima aliopewa binadamu na Mungu, na dhihirisho kwamba maisha yalikuja kutoka Kwake. Ingawa watu wengi wanaweza kukosa kuamini kwamba maisha yalitoka kwa Mungu, binadamu bila ya kufahamu hufurahia yote yatokayo kwa Mungu, iwe wanaamini au wanakana uwepo Wake. Iwapo siku moja Mungu kwa ghafla Atabadili moyo na Atake kurudisha yote yaliyomo duniani na kuchukua maisha Aliyotoa, basi yote duniani yataisha. Mungu hutumia maisha Yake kukimu vitu vyote vilivyo hai na visivyo na uhai, na kuleta yote kwa utaratibu mzuri kwa mujibu wa uwezo na mamlaka Yake. Huu ni ukweli ambao hauwezi kuwazika au kueleweka na yeyote, na kweli hizi zisizoeleweka kwa fikira zetu ni dhihirisho halisi na ushahidi wa nguvu za Mungu katika maisha. Sasa hebu nikupe siri: Ukuu wa uzima wa Mungu na nguvu ya uzima Wake haziwezi kueleweka na kiumbe yeyote. Hivi ndivyo hali ilivyo sasa, kama ilivyokuwa awali, na itakuwa hivyo wakati ujao. Siri ya pili Nitakayotoa ni

hii: Chanzo cha uhai hutoka kwa Mungu, kwa viumbe wote, bila kujali jinsi wanavyoweza kuwa tofauti katika maumbile au muundo. Hata uwe kiumbe hai wa aina gani, huwezi kwenda kinyume na njia ya maisha ambayo Mungu ameweka. Katika hali yoyote, kile Napenda ni kuwa mwanadamu kuelewa hili: Bila ulinzi, utunzaji, na utoaji wa Mungu, mwanadamu hawezi kupokea yote aliyokusudiwa kupokea, haijalishi anajaribu kwa juhudi au kupambana kwa bidii namna gani. Bila ruzuku ya uhai kutoka kwa Mungu, mwanadamu hupoteza maana ya thamani ya kuishi na madhumuni ya maana katika maisha. Mungu angewezaje kumruhusu mwanadamu, ambaye bila umakini hupoteza thamani ya uhai wake, kuishi hivyo bila ya kujali? Kama vile nimesema awali: Usisahau kwamba Mungu Ndiye chanzo cha maisha yako. Iwapo mwanadamu atashindwa kuthamini yote ambayo Mungu Amemfanyia, Mungu Hatachukua tu kile Alichotoa mbeleni pekee, lakini Atatoza, kutoka kwa binadamu kama fidia, thamani ya yote ambayo Ametoa mara mbili.

Mei 26, 2003

Kutanafusi kwa Mwenye Uweza

Kunayo siri kubwa moyoni mwako, ambayo hujawahi kuifahamu kamwe, kwa sababu umekuwa ukiishi katika ulimwengu bila mwanga. Moyo wako na roho yako vimepokonywa na yule mwovu. Macho yako yamezuiwa kwa giza yasione, na huwezi kuliona jua angani wala nyota ikimetameta wakati wa usiku. Masikio yako yamezibwa na maneno ya udanganyifu, na husikii sauti ya Yehova ingurumayo kama radi, wala sauti ya maji yakitiririka kutoka katika kiti cha enzi. Umepoteza kila kitu ambacho kilipaswa kuwa chako kwa haki, kila kitu ambacho Mwenye uweza alikupa. Umeingia katika bahari ya mateso isiyokuwa na mwisho, bila nguvu ya kukuokoa, bila matumaini ya kurudi ukiwa hai, na yote unayofanya ni kupambana na kusonga kila siku.... Tokea wakati huo, hungeweza kuepuka kuteswa na yule mwovu, uliwekwa mbali na baraka za mwenye Uweza, mbali na kukimu kwa mwenye Uweza, unatembea katika njia ambayo huwezi kurejea nyuma tena. Kuitwa mara milioni hakuwezi kulisimua moyo wako na roho yako. Unalala fofofu mikononi mwa yule mwovu, ambaye amekushawishi katika ulimwengu usio na mipaka, bila mwelekeo na bila alama za barabarani. Tokea hapo, umepoteza hali yako ya asili ya kutokuwa na hatia na utakatifu wako, na kuanza kujificha kutokana na utunzaji wa mwenye Uweza. Ndani ya moyo wako, yule mwovu anakuelekeza katika kila jambo na anakuwa uhai wako. Humwogopi tena, kumwepuka, au kumshuku; badala yake, unamchukulia kama Mungu aliye moyoni mwako. Unanza kumtukuza na kumwabudu, na nyinyi wawili mnakuwa msiotengana kama mwili na kivuli chake, kila akitoa nafsi yake kwa mwingine katika uzima na mauti. Hujui lolote kabisa kuhusu mahali ulikotoka, kwa nini ulizaliwa, au kwa nini utakufa. Unamtazama Mwenye uweza kama mgeni; hujui mwanzo Wake,

sembuse yale yote ambayo Amekutendea. Kila kitu kitokacho Kwake kimekuwa cha kuchukiza kwako. Huvitunzi wala kujua thamani yavyo. Unatembea kando na yule mwovu, kuanzia siku ile ulipoanza Mwenye uweza alianza kukukimu. Wewe na yule mwovu mmepitia maelfu ya miaka ya dhoruba na tufani pamoja, na pamoja naye, mnampinga Mungu ambaye alikuwa chanzo cha uhai wako. Hujui lolote kuhusu kutubu, sembuse kwamba umefikia ukingo wa kuangamia. Unasahau kwamba yule mwovu amekujaribu na kukutesa; umesahau asili yako. Kwa njia hii, yule mwovu amekuwa akikuharibu, hatua baada ya hatua, hata mpaka leo. Moyo wako na roho yako vimekufa ganzi na vimeoza. Umeacha kulalamika juu ya maudhi ya dunia ya wanadamu, na huamini tena kwamba dunia si ya haki. Bado hujali sana kama Mwenye uweza yupo. Hii ni kwa sababu ulimchukulia yule mwovu kuwa baba yako wa kweli kitambo, na huwezi tena kutengana naye. Hii ndiyo siri iliyo moyoni mwako.

Alfajiri inapofika, nyota ya asubuhi inaanza kuangaza mashariki. Hii ni nyota ambayo haijawahi kuwepo hapo awali. Inaliangaza anga lililo bado na nyota, ikikuwasha nuru iliyozimwa katika mioyo ya wanadamu. Binadamu si wapweke tena, kwa sababu ya mwanga huu, ambao hukuangazia wewe sawia na wengine. Lakini ni wewe tu unayebaki ukiwa umelala fofofo katika usiku wa giza. Huwezi kuisikia sauti, wala kuiona nuru, hujui kuhusu ujio wa mbingu mpya na nchi mpya, enzi mpya, kwa sababu baba yako hukwambia, “Mwanangu, usiamke, bado ni mapema. Hali ya anga ni baridi, kwa hivyo usiende nje, usije ukachomwa machoni kwa mkuki na upanga.” Unaamini maonyo ya baba yako pekee, maana unaamini kwamba baba yako tu ndiye yuko sahihi, kwa sababu baba yako ana umri mkubwa kuliko wewe na kwamba baba yako anakupenda sana. Maonyo kama hayo na upendo kama huo unakufanya uwache kuamini hekaya kwamba kuna nuru ulimwenguni, na uwache kujali kama ukweli bado upo ulimwenguni humu. Huthubutu tena kutumainia ukombozi kutoka kwa mwenye Uweza. Umeridhika kuwa katika hali hiyo, hutumainii tena ujio wa nuru, na hutazamii tena kuja kwa Mwenye uweza kama ilivyo katika hekaya. Inavyokuhusu wewe, yote yaliyo mazuri hayawezi kufufuliwa tena, wala hayawezi kuendelea kuwepo. Kesho ya wanadamu, siku za baadaye za wanadamu zinapotea, zinaharibika kabisa machoni pako. Unayashika sana mavazi ya baba yako kwa nguvu zako zote, ukifurahia kushiriki taabu zake, ukihofu sana kumpoteza mwenzako wa kusafiri na mwelekeo wa safari yako ya mbali. Ulimwengu huu mkubwa na wenye giza wa binadamu umewaunda wengi wenu, kuwa majasiri na watu wa kujitahidi sana katika kutekeleza majukumu mbalimbali ya ulimwengu huu. Umewaunda “mashujaa” wengi ambao hawaogopi kifo kabisa. Zaidi ya hayo, umetengeneza kundi baada ya kundi la watu waliokufa ganzi na wanadamu waliopooza ambao hawajui makusudi ya kuumbwa kwao. Macho ya Mwenye uweza hukagua kila mmoja wa jamii ya wanadamu walio katika mateso makali. Anachosikia ni vilio vya wale wanaoteseka, Anachoona ni kutokua kwa aibu kwa wale wanaoteseka, na Anachohisi

ni kutojiweza na hofu ya jamii ya wanadamu ambayo imepoteza neema ya wokovu. Wanadamu wanakataa utunzaji Wake, wakichagua kutembea katika njia yao wenyewe, na wakijaribu kukwepa macho Yake yanayochunguza kwa karibu, wakiona ni afadhali waonje uchungu wa kilindi cha bahari hadi mwisho, pamoja na adui. Kutanafusi kwa Mwenye uweza hakisikiki tena na binadamu. Mikono ya Mwenye uweza haiko tayari kuwapapasa tena wanadamu hawa wenye huzuni. Anarudia kazi Yake, mara kwa mara akikamata tena, na mara kwa mara akipoteza tena, na kutoka wakati huo, Yeye anaaanza kuchoka, kujihisi mchovu, na hivyo Anasitisha kazi inayofanyika, na kuwacha kutembea kati ya wanadamu.... Wanadamu hawana ufahamu kabisa kuhusu mabadiliko haya, hawajui kuhusu kuja na kuondoka, huzuni na ghamu ya Mwenye uweza.

Yote yaliyo duniani humu yanabadilika haraka sawasawa na mawazo ya Mwenye uweza, na chini ya macho Yake. Mambo ambayo wanadamu hawajawahi kuyasikia yanaweza kuja kwa ghafla, ilhali vitu ambavyo wanadamu wamemiliki kwa muda mrefu vinaweza kutoweka bila wao kujua. Hakuna anayeweza kutambua mahali alipo Mwenye uweza sembuse yeyote kuweza kuhisi kuzidi uwezo wa mwanadamu na ukuu wa nguvu za uzima za Mwenye uweza. Anazidi uwezo wa mwanadamu kwa vile Anavyoweza kufahamu yale ambayo wanadamu hawawezi. Yeye ni mkuu kwa vile ni Yeye anayekataliwa na wanadamu na bado Anawaokoa wanadamu. Yeye anajua maana ya maisha na mauti na, isitoshe, Anajua ni kanuni gani zinazofaa katika kuongoza uwepo wa wanadamu Aliowaumba. Yeye ndiye msingi ambao kwao uwepo wa wanadamu hutegemea, na ndiye Mkombozi ambaye hufufua wanadamu tena. Yeye huilemea mioyo yenye furaha kwa huzuni na kuiinua mioyo yenye huzuni kwa furaha, yote kwa ajili ya kazi Yake, na kwa ajili ya mpango Wake.

Wanadamu, baada ya kuuwacha utoaji wa uzima kutoka kwa Mwenye uweza, hawajui azma ya kuishi, lakini hata hivyo wanaogopa kifo. Hawana usaidizi wala msaada, lakini bado wanasita kufumba macho yao, na wanajitayarisha kuendeleza uwepo wa aibu ulimwenguni humu, magunia ya miili wasio na hisia za roho zao wenyewe. Unaishi hivi, bila matumaini, kama vile wafanyavyo wengine, bila lengo. Kuna aliye Mtakatifu tu katika hekaya atakayekuja kuwaokoa watu ambao, wakiwa wanapiga kite katika mateso yao, wanatamani sana kufika Kwake. Hadi sasa, imani hii haijafikiwa kwa wale ambao hawana fahamu. Hata hivyo, watu bado wanaitaka sana. Mwenye uweza ana rehema kwa watu hawa ambao wameteseka sana. Wakati uo huo, Amechoshwa na watu hawa wasio na fahamu, maana imembidi Asubiri sana kupata jibu kutoka kwa wanadamu. Anatamani kutafuta, kuutafuta moyo wako na roho yako, kukuletea chakula na maji na kukuzindua, ili usione kiu na kuhisi njaa tena. Unapokuwa umechoka na unapoanza kuhisi huzuni kubwa ya ulimwengu huu, usipotoke, usilie. Mwenyezi Mungu, Mlinzi, atakaribisha kuwasili kwako wakati wowote. Yuko kandokando yako akiangalia, akikusubiri

urudi. Anasubiri siku ambayo utarudisha ghafla kumbukumbu yako: ukitambua ukweli kwamba ulitoka kwa Mungu, lakini wakati fulani usiojulikana ukapoteza mwelekeo wako, wakati fulani usiojulikana ukaanguka barabarani ukiwa hujitambui na tena wakati fulani usiojulikana ukampata “baba.” Isitoshe, unagundua kuwa Mwenye uweza amekuwa hapo muda huo wote, akiangalia, akisubiri kurejea kwako, kwa muda mrefu sana. Amekuwa akitazama na tamanio kubwa, Akingoja itiko pasipo jibu. Kusubiri Kwake kunazidi thamani, na ni kwa ajili ya moyo na roho ya wanadamu. Pengine kusubiri huku hakuna mwisho, na pengine kumefikia mwisho. Lakini unapaswa kujua moyo wako na roho yako hasa viko wapi sasa hivi.

Mei 28, 2003

Kuonekana kwa Mungu Kumeleta Enzi Mpya

Mpango wa Mungu wa miaka elfu sita ya usimamizi unaisha, na lango la ufalme limefunguliwa kwa wale ambao wanatafuta kuonekana kwa Mungu. Ndugu wapendwa, mnasubiri nini? Mnatafuta nini? Mnasubiri kuonekana kwa Mungu? Mnazitafuta nyayo za Mungu? Kuonekana kwa Mungu kunatamaniwa sana! Ni vigumu, kiasi gani kupata nyayo za Mungu! Katika enzi kama hii, katika dunia kama hii, lazima tufanye nini ili tushuhudie kuonekana kwa Mungu? Sharti tufanye nini ili tufuate nyayo za Mungu? Wale wote wanaosubiri kuonekana kwa Mungu wanakumbana na maswali kama haya. Nyinyi nyote mmewahi kuyafikiria zaidi ya mara moja—ila matokeo ni gani? Mungu hujidhihirisha wapi? Nyayo za Mungu zipo wapi? Mmepata majibu? Majibu ya watu wengi yangekuwa: Mungu hudhihirika miongoni mwa wale wanaomfuata na nyayo Zake zimo miongoni mwetu; ni rahisi hivyo! Mtu yeyote anaweza kutoa jibu kwa kutumia mbinu fulani, lakini je, mnaifahamu kuonekana kwa Mungu ni nini, na nyayo za Mungu ni nini? Kuonekana kwa Mungu hurejelea kuwasili Kwake duniani kufanya kazi Yake. Akiwa na utambulisho na tabia Yake, na katika njia ambayo ni ya asili Kwake, Yeye hushuka miongoni mwa wanadamu kufanya kazi ya kuanzisha enzi mpya na kukamilisha enzi nyingine. Kuonekana kwa aina hii si aina fulani ya sherehe. Si ishara, picha, muujiza, au ono kuu, na hata zaidi si mchakato fulani wa kidini. Ni ukweli halisi ambao waweza kushikwa na kuonekana. Kuonekana kama huku si kwa ajili ya kufuata taratibu, au kwa ajili ya shughuli ya muda mfupi; ni, badala yake, kwa ajili ya hatua ya kazi ya mpango Wake wa usimamizi. Kuonekana kwa Mungu daima ni kwenye maana na daima huenda pamoja na mpango wa usimamizi. Kuonekana huku ni tofauti kabisa na udhihirisho wa uongozi wa Mungu, utawala na kupata nuru kwa mwanadamu. Mungu hufanya kazi kubwa kila mara Anapojifunua. Kazi hii ni tofauti na enzi yoyote nyingine. Haiwezi kufikirika na mwanadamu na haijawahi kupitiwa mwanadamu. Ni kazi ambayo huanzisha enzi mpya na kutamatisha enzi ya awali, na ni aina mpya ya kazi na iliyoboreshwa kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu; aidha, ni kazi ya

kuleta wanadamu katika enzi mpya. Huo ndio umuhimu wa kuonekana kwa Mungu.

Katika wakati uo huo wa kuelewa kuonekana kwa Mungu, mnapaswa kutafuta nyayo za Mungu vipi? Swali hili si gumu kueleza: Palipo na kuonekana kwa Mungu; mtapata nyayo za Mungu. Maelezo kama haya yanaonekana yapo wazi sana, ila si rahisi kutekeleza kwani watu wengi hawafahamu pale Mungu anapojidhihirisha, wala pale ambapo Angependa kujidhihirishia ama iwapo Anapaswa kujidhihirisha. Wengine kwa msukumo huamini kuwa palipo na kazi ya Roho Mtakatifu kuna kuonekana kwa Mungu. Ama sivyo watu huamini kuwa palipo na watu mashuhuri wa kiroho ndipo Mungu huonekana. Vinginevyo, wanaamini kuwa palipo na watu wanaojulikana vyema ndipo Mungu huonekana. Kwa sasa tusishauriane ikiwa imani hizi ni sahihi au la. Kujibu swali kama hilo, kwanza ni lazima tuwe wazi kuhusu lengo: tunazitafuta nyayo za Mungu. Hatutafuti viongozi wa kiroho, wala kutafuta watu mashuhuri; tunafuata nyayo za Mungu. Kwa hivyo, kwa kuwa tunatafuta nyayo za Mungu, ni sharti tufuate mapenzi ya Mungu, maneno ya Mungu, matamshi ya Mungu—kwani palipo na maneno mapya ya Mungu, kuna sauti ya Mungu, na palipo na nyayo za Mungu, pana matendo ya Mungu. Palipo na maonyesho ya Mungu pana kuonekana kwa Mungu, na palipo na kuonekana kwa Mungu, pana ukweli, njia na uzima. Mlipokuwa ukitafuta nyayo za Mungu, mliyapuuza maneno haya kuwa “Mungu ndiye ukweli, njia na uzima.” Kwa hivyo, watu wengi wanapoupokea ukweli, hawaamini kuwa wamepata nyayo za Mungu na hata zaidi hawasadiki kuonekana kwa Mungu. Kosa hilo ni kuu kiasi gani! Kuonekana kwa Mungu hakuwezi kulinganishwa na fikira za mwanadamu, sembuse Mungu kuonekana kwa amri ya mwanadamu. Mungu hufanya uamuzi Wake mwenyewe na huwa na mipango Yake Afanyapo kazi; aidha, Ana malengo Yake, na mbinu Zake. Si lazima Ajadiliane kazi Azifanyazo na mwanadamu au Atafute ushauri wa mwanadamu, sembuse kumfahamisha kila mtu kuhusu kazi Yake. Hii ndiyo tabia ya Mungu na, zaidi ya hayo, inafaa kutambuliwa na kila mmoja. Kama mnatamani kushuhudia kuonekana kwa Mungu, kama mnatamani kufuata nyayo za Mungu, basi kwanza ni sharti mzishinde dhana zenu. Ni sharti muache kudai kuwa Mungu afanye hiki au kile sembuse kumweka Yeye ndani ya mipaka yenu wenyewe na kumwekea upeo kwa dhana zenu. Badala yake, mnafaa kujua ni vipi mtazitafuta nyayo za Mungu, na vipi mnapaswa kukubali kuonekana kwa Mungu na ni vipi mnapaswa kutii kazi mpya ya Mungu; hiki ndicho kinapaswa kufanywa na mwanadamu. Kwa kuwa mwanadamu si ukweli, na hamiliki ukweli, mwanadamu anafaa kutafuta, kukubali na kutii.

Bila kujali kama wewe ni Mmarekani, Mwingereza, au mtu wa taifa jingine, ni lazima utoke nje ya mipaka yako, ni lazima ujipite, na ni sharti uione kazi ya Mungu kama kiumbe wa Mungu. Kwa njia hii, hutaweka vikwazo katika nyayo za Mungu. Kwa sababu, leo, watu hufikiri kuwa haiwezekani Mungu kudhihirika katika nchi au taifa fulani. Umuhimu wa kazi ya Mungu una undani kiasi gani, na kuonekana kwa Mungu kuna maana ilioje! Vinawezaje kupimwa kwa

dhana na fikira za mwanadamu? Na ndiyo maana Ninasema kuwa unafaa kujiondoa katika dhana za uraia wako au kabila lako unapokutafuta kuonekana kwa Mungu. Kwa njia hii, hutafungwa na dhana zako mwenyewe; kwa njia hii, utahitimu kukaribisha kuonekana kwa Mungu. Vinginevyo, daima utakuwa gizani na hutapata kibali cha Mungu.

Mungu ni Mungu wa wanadamu wote. Hawi mali binafsi ya nchi au taifa lolote na hufanya kazi ya mpango Wake bila kuzuiwa na mfumo wowote, nchi au taifa. Labda hujawahi kuwazia mfumo huu, au labda wewe hukana kuwepo kwake, au labda nchi au taifa ambapo Mungu huonekana limebaguliwa na lina maendeleo duni sana duniani. Na bado Mungu ana busara Yake. Na uwezo Wake kupitia ukweli na tabia Zake kwa hakika Amepata kundi la watu wenye mawazo sawa na Yeye. Na Amepata kundi la watu ambao alitaka kutengeneza: kundi lililoshindwa Naye, watu ambao wameyavumilia majaribu machungu na aina zote za mateso na wanaweza kumfuata mpaka mwisho. Malengo ya kuonekana kwa Mungu, bila vizuizi vya nchi yoyote, ni kumruhusu Akamilishe kazi ya mpango Wake. Kwa mfano, Mungu alipopata mwili kule Uyahudi, lengo Lake lilikuwa kutimiza kazi ya msalaba na kuwakomboa wanadamu wote. Na bado Wayahudi waliamini kuwa Mungu asingeweza kulifanya hili, na wakafikiri kuwa Mungu asingeweza kuwa mwili na kuchukua umbo la Bwana Yesu. “Kutowezekana” kwao kukawa msingi wa kumshutumu na kumpinga Mungu na hatimaye ikawa kuangamizwa kwa Israeli. Leo hii, watu wengi wamefanya kosa lile lile. Wanatangaza kuonekana kwa Mungu ambako kumekaribia, na vilevile kukushutumu kuonekana huku; “kutowezekana” kwao kwa mara nyingine kunabana kuonekana kwa Mungu katika mipaka ya dhana zao. Na kwa hivyo Nimeona watu wengi wakicheka na kuanguka baada ya kuyasikia maneno ya Mungu. Kicheko hiki kinatofautianaje na shutuma na kukufuru kwa Wayahudi? Hamna moyo wa dhati katika kukabiliana na ukweli, sembuse kutamani ukweli. Nyinyi huchunguza tu kama vipofu na kusubiri kwa utepetevu. Mtajifaidi na nini kwa kutafiti na kusubiri kwa njia hii? Je, mnaweza kupata uongozi binafsi wa Mungu? Kama huwezi kuyang’amua matamshi ya Mungu, umehitimu vipi kushuhudia kuonekana kwa Mungu? Mahali ambapo Mungu anajitokeza, kuna maonyesho ya kweli, na kuna sauti ya Mungu. Ni wale tu wanaoukubali ukweli ndio watakaoisikia sauti ya Mungu, na ni hao tu waliowezechwa kushuhudia kuonekana kwa Mungu. Weka dhana zako kando. Tafakari na kusoma maneno haya kwa makini. Ukitamani ukweli, Mungu atakupaa nuru ya kuyafahamu mapenzi Yake na maneno Yake. Wekeni kando mitazamo yenu ya “haiwezekani”! Kadiri watu wanavyozidi kuamini kuwa jambo fulani haliwezekani, ndivyo uwezekano wa utukiaji wake unavyoendelea kujiri, kwani ufahamu wa Mungu hupaa juu kuliko mbingu, mawazo ya Mungu yako juu ya yale ya mwanadamu, na kazi ya Mungu inapita mipaka ya fikira za mwanadamu. Kadiri kitu kinavyokuwa hakiwezekani, ndivyo kunavyokuwepo na ukweli wa kutafutwa; kadiri kitu kilivyo nje ya mipaka ya dhana na fikira za mwanaadamu,

ndivyo kinavyozidi kuwa na mapenzi ya Mungu. Kwani bila kujali Mungu anajidhihirishia wapi, Mungu bado ni Mungu, na kiini chake hakitawahi kubadilika kwa sababu ya mahali ama namna ya kuonekana Kwake. Tabia ya Mungu hubaki kuwa vilevile bila kujali nyayo Zake ziko wapi. Bila kujali nyayo za Mungu zilipo, Yeye ndiye Mungu wa wanadamu wote. Kwa mfano, Bwana Yesu si Mungu tu wa Waisraeli, lakini vilevile ni Mungu wa watu wote wa Asia, Ulaya, na Marekani, na hata zaidi, ndiye Mungu pekee wa ulimwengu mzima. Hivyo basi, tuyatafute mapenzi ya Mungu na tugundue kuonekana Kwake kutoka kwa matamshi Yake na tufuate nyayo Zake. Mungu ndiye ukweli, njia na uzima. Maneno Yake na kuonekana Kwake yanakuwepo sawia, na tabia na nyayo Zake daima zitapatikana na wanadamu. Ndugu wapendwa, natumaini kwamba mnaweza kuona kuonekana kwa Mungu katika maneno haya, na kwamba muanze kuzifuata nyayo Zake kuelekea enzi mpya, na hadi katika mbingu mpya yenye kupendeza na dunia mpya iliyoandaliwa kwa wale wanaosubiri kuonekana kwa Mungu.

Mungu Anaongoza Majaliwa ya Wanadamu Wote

Kama washiriki wa jamii ya binadamu na Wakristo wamchao Mungu, ni jukumu na wajibu wa sisi wote kutoa akili na mwili wetu kwa kutimiza agizo la Mungu, kwani uhai wetu wote ulitoka kwa Mungu, na upo kwa sababu ya ukuu wa Mungu. Kama akili zetu na miili yetu si kwa ajili ya agizo la Mungu na si kwa sababu ya kusudi la haki la mwanadamu, basi nafsi zetu hazina thamani kwa wale waliokufa kishahidi kwa ajili ya agizo la Mungu, na thamani ndogo zaidi kwa Mungu, aliyetupa kila kitu.

Mungu aliumba dunia hii, Aliumba mwanadamu huyu, na zaidi ya hayo Alikuwa muasisi wa utamaduni wa zamani wa Giriki na ustaarabu wa binadamu. Ni Mungu tu anayemfariji huyu mwanadamu, na ni Mungu tu anayemtunza mwanadamu huyu usiku na mchana. Ukuaji na maendeleo ya binadamu hayatengani na ukuu wa Mungu, na historia na mustakabali wa mwanadamu ni zisizochangulika kutoka kwa miundo ya Mungu. Kama wewe ni Mkristo wa kweli, basi hakika utaamini kwamba kupanda na kushuka kwa nchi ama taifa lolote hufanyika kulingana na miundo ya Mungu. Mungu pekee hujua majaliwa ya nchi ama taifa, na Mungu pekee hudhibiti mwendo wa huyu mwanadamu. Iwapo mwanadamu anataka kuwa na majaliwa mazuri, iwapo nchi inataka kuwa na majaliwa mazuri, basi lazima mwanadamu ampigie Mungu magoti kwa ibada, atubu na kukiri mbele ya Mungu, la sivyo majaliwa na hatima ya mwanadamu hayataepuka kumalizika kwa janga.

Angalia nyuma wakati wa safina ya Nuhu: Wanadamu walikuwa wapotovu sana, walikuwa wamepotea kutoka katika baraka za Mungu, hawakuwa wanatunzwa na Mungu tena, na walikuwa wamepoteza ahadi za Mungu. Waliishi gizani, bila mwangaza wa Mungu. Hivyo wakawa waasherati kwa asili, wakajiachilia katika mkengeuko wa kutisha. Watu kama hao

hawangeweza tena kupokea ahadi za Mungu; hawakufaa kushuhudia uso wa Mungu, wala kusikia sauti ya Mungu, kwani walikuwa wamemwacha Mungu, kuweka kando yote Aliyowapa, na kusahau mafunzo ya Mungu. Mioyo yao ilipotea mbali zaidi na zaidi na Mungu, na ilivyofanya hivyo, wakawa wapotovu zaidi ya mantiki na ubinadamu wote na wakazidi kuwa waovu. Hivyo walikaribia kifo zaidi, na kukabiliwa na ghadhabu na adhabu ya Mungu. Ni Nuhu tu aliyemwabudu Mungu na kuepukana na uovu, na hivyo aliweza kusikia sauti ya Mungu, na kusikia maelekezo ya Mungu. Alijenga safina kulingana na maelekezo ya neno la Mungu, na kukusanya aina yote ya viumbe hai. Na kwa njia hii, wakati kila kitu kilikuwa kimetayarishwa, Mungu aliangamiza dunia. Nuhu tu na wanachama saba wa familia yake walinusurika maangamizi, kwani Nuhu alimwabudu Yehova na kuepukana na uovu.

Kisha angalia enzi ya sasa: Hawa watu wenye haki kama Nuhu, ambao wangeweza kumwabudu Mungu na kuepuka uovu, wamekoma kuwepo. Lakini bado Mungu ana fadhili kwa mwanadamu huyu, na Anamsamehe mwanadamu wakati huu wa enzi ya mwisho. Mungu anawatafuta wanaomtaka Yeye ajitokeze. Anawatafuta wale wanaoweza kuyasikia maneno Yake, wale ambao hawajasahau agizo Lake na wanatoa mioyo na miili yao Kwake. Anawatafuta wale walio watiifu kama watoto wachanga mbele Yake, na hawampingi. Kama hujazuiliwa na nguvu zozote katika ibada yako Kwake, basi Mungu atakutazama na neema, na kukupea baraka Zake. Kama wewe ni wa daraja la juu, wa sifa ya heshima, aliyemiliki maarifa mengi, mmiliki wa mali nyingi, na kuungwa mkono na watu wengi, lakini mambo haya hayakuzuii kuja mbele za Mungu kuukubali wito Wake na agizo Lake, kufanya kile Mungu anachokuambia ufanye, basi yote unayoyafanya yatakuwa yenye umuhimu zaidi duniani na yenye haki zaidi ya binadamu. Ukiukataa wito wa Mungu kwa sababu ya hadhi yako na malengo yako mwenyewe, yote utakayoyafanya yatalaaniwa na hata kudharauliwa na Mungu. Labda wewe ni rais, ama mwanasayansi, ama mchungaji, ama mzee, lakini bila kujali ukuu wa ofisi yako, ukitegemea maarifa yako na uwezo katika shughuli zako, basi daima utakuwa wa kushindwa na kamwe utanyimwa baraka za Mungu, kwa sababu Mungu hakubali chochote unachofanya, na Hakubali kwamba kazi yako ni yenye haki, wala kukubali kwamba unafanya kazi kwa msaada wa mwanadamu. Atasema yote unayofanya, ni ya kutumia maarifa na nguvu za mwanadamu kumvulia mwanadamu ulinzi wa Mungu na kumnyima baraka za Mungu. Atasema kuwa unamwongoza mwanadamu kuelekea gizani, kuelekea kifo, na kuelekea mwanzo wa kuwepo bila mipaka ambapo mwanadamu amempoteza Mungu na baraka Zake.

Kutoka wakati mwanadamu kwanza alikuwa na sayansi ya jamii, akili yake ilishughulishwa na sayansi na maarifa. Kisha sayansi na maarifa vikawa vyombo vya kutawala mwanadamu, na hapakuwa tena na nafasi ya kutosha kumwabudu Mungu, na hapakuwa tena na mazingira mazuri ya kumwabudu Mungu. Nafasi ya Mungu ikashuka hata chini zaidi moyoni mwa mwanadamu.

Dunia moyoni mwa mwanadamu bila nafasi ya Mungu ni giza, tupu bila matumaini. Na hivyo kukatokea wanasayansi wa jamii, wataalamu wa historia na wanasiasa wengi kueleza nadharia ya sayansi ya jamii, nadharia ya mageuko ya binadamu, na nadharia nyingine zinazopinga ukweli kwamba Mungu alimuumba mwanadamu, kujaza moyo na akili ya mwanadamu. Na kwa njia hii, wanaoamini kwamba Mungu aliumba kila kitu wanakuwa wachache zaidi, na wale wanaoamini nadharia ya mageuko wanakuwa hata wengi kwa nambari. Watu zaidi wanachukulia rekodi za kazi ya Mungu na maneno Yake wakati wa enzi ya Agano la Kale kuwa hadithi na hekaya. Kwa mioyo yao, watu wanakuwa wasiojali heshima na ukubwa wa Mungu, kwa imani kwamba Mungu yupo na anatawala kila kitu. Kusalia kwa mwanadamu na majaliwa ya nchi na mataifa si muhimu kwao tena. Mwanadamu anaishi katika dunia tupu akijishughulisha tu na kula, kunywa, na ufuatiliaji wa furaha. ... Watu wachache wanashughulika kutafuta Afanyapo Mungu kazi Yake leo, ama kutafuta jinsi Anavyoongoza na kupanga majaliwa ya mwanadamu. Na kwa njia hii, ustaarabu wa ubinadamu bila fahamu ukawa huwezi kukutana na matakwa ya mwanadamu hata zaidi, na hata kuna watu zaidi wanaohisi kwamba, kuishi kwa dunia kama hii, wanayo furaha ya chini kuliko watu walioenda. Hata watu wa nchi zilizokuwa na ustaarabu wa juu wanaeleza malalamiko haya. Kwani bila mwongozo wa Mungu, bila kujali jinsi viongozi na wanasosiolojia wanatafakari kuhifadhi ustaarabu wa binadamu, haina mafanikio. Hakuna anayeweza kujaza utupu kwa moyo wa mwanadamu, kwani hakuna anayeweza kuwa uhai wa mwanadamu, na hakuna nadharia ya kijamii inayoweza kumwoko kutokana na utupu unaomtesa. Sayansi, maarifa, uhuru, demokrasia, wasaa wa mapumziko, faraja, haya yote ni mapumziko ya muda, Hata na mambo haya, mwanadamu hataepuka kufanya dhambi na kuomboleza udhalimu wa jamii. Mambo haya hayawezi kupunguza tamaa ya mwanadamu na hamu ya kuchunguza. Kwa sababu mwanadamu aliumbwa na Mungu na kafara na uchunguzi usio na sababu wa mwanadamu vitamwongoza tu kwa dhiki zaidi. Mwanadamu daima atakuwa katika hali ya hofu isiyoisha, hatajua jinsi ya kuukabili mustakabali wa wanadamu, ama jinsi ya kuikabili njia iliyo mbele. Mwanadamu atakuja hata kuogopa sayansi na elimu, na kuhofia hata zaidi utupu ulio ndani yake sana. Duniani humu, bila kujali kama unaishi katika nchi huru ama isiyo na haki za binadamu, huwezi kabisa kuponyoka majaliwa ya mwanadamu. Kama wewe ni kiongozi ama anayeongozwa, huwezi kabisa kuponyoka hamu ya kuchunguza majaliwa, siri na majaliwa ya mwanadamu. Chini ya hayo, huna uwezo wa kutoroka hisia ya utupu inayotatiza. Matukio kama haya, yaliyo kawaida kwa wanadamu wote, yanaitwa matukio ya kijamii na wanasosiolojia, lakini hakuna mtu mkubwa anayeweza kuja mbele kutatua shida kama hizi. Mwanadamu, hata hivyo, ni mwanadamu. Nafasi na maisha ya Mungu hayawezi kubadilishwa na mwanadamu yeyote. Mwanadamu hahitaji tu jamii iliyo na haki, ambapo kila mtu analishwa vyema na ana uhuru na usawa, lakini wokovu wa Mungu na Yeye kuwapa uhai. Wakati tu mwanadamu atapokea wokovu wa Mungu na kupatiwa uhai na Yeye ndipo mahitaji, hamu ya

kuchunguza, na utupu wa kiroho wa mwanadamu utaweza kutatuliwa. Iwapo watu wa nchi ama taifa hawawezi kupokea wokovu na utunzaji wa Mungu, basi nchi ama taifa kama hilo litatembelea njia inayoelekea uharibifuni, inayoelekea gizani, na litaangamizwa na Mungu.

Labda nchi yako inafanikiwa sasa, lakini ukiruhusu watu wako kupotea kutoka kwa Mungu, basi nchi yako itazidi kujipata bila baraka za Mungu. Ustaarabu wa nchi yako utazidi kukanyagiwa chini, na kabla ya muda mrefu watu watamwasi Mungu na kulaani Mbingu. Na hivyo, bila kujulikana kwa mwanadamu, majaliwa ya nchi yataletwa kwa uharibifu. Mungu ataziinua nchi zenye nguvu ili kukabiliana na nchi hizo zilizolaaniwa na Mungu, na anaweza hata kuzifuta kutoka uso wa dunia. Kupanda na kushuka kwa nchi ama taifa kunategemea kama viongozi wao wanamwabudu Mungu, na kama wanawaongoza watu wao karibu na Mungu na kumwabudu. Lakini, kwa hii enzi ya mwisho, kwa sababu wale wanaomtafuta Mungu kwa kweli na kumwabudu wanazidi kuwa wachache, Mungu anaweka fadhili ya pekee juu ya nchi ambapo Ukristo ni dini ya serikali. Anazikusanya pamoja kuunda kambi ya haki kiasi ya dunia, wakati nchi zikanazo Mungu ama zile zisizomwabudu Mungu wa kweli zinakuwa wapinzani wa kambi ya haki. Kwa njia hii, Mungu hana tu mahali miongoni mwa wanadamu pa kufanyia kazi Yake, lakini pia Anapata nchi zinazoweza kutumia mamlaka ya haki, ili kulazimisha mipaka na vikwazo kwa nchi hizo zinazompinga Mungu. Lakini licha ya hayo, bado hakuna watu zaidi wanaokuja mbele kumwabudu Mungu, kwa sababu mwanadamu amepotea mbali sana kutoka Kwake, na Mungu hajakuwa kwa mawazo ya mwanadamu kwa muda mrefu. Kunabakia tu duniani nchi zinazotumia haki na kupinga udhalimu. Lakini hii ni mbali na matakwa ya Mungu, kwani hakuna kiongozi wa nchi yoyote atamruhusu Mungu kuongoza watu wake, na hakuna chama cha kisiasa kitakachokusanya pamoja watu wake kumwabudu Mungu; Mungu amepoteza mahala Pake halali kwa mioyo ya nchi zote, taifa, chama tawala, na hata kwa moyo wa kila mtu. Ingawa nguvu za haki ziko kwa dunia hii, utawala ambapo Mungu hana mahali kwa moyo wa mwanadamu ni dhaifu. Bila baraka ya Mungu, uwanja wa kisiasa utaanguka katika vurugu na wenye kuweza kudhuriwa na mashambulizi. Kwa mwanadamu, kuwa bila baraka ya Mungu ni kama kuwa bila jua. Bila kujali jinsi viongozi wanafanya mchango kwa watu wao kwa uangalifu, bila kujali idadi ya mikutano ya haki wanadamu wanafanya pamoja, hakuna kati ya hii itakayorejesha mambo ama kubadilisha majaliwa ya mwanadamu. Mwanadamu anaamini kuwa nchi ambapo watu wanalishwa na kuvalishwa nguo, ambapo watu wanaishi kwa amani, ni nchi nzuri, na iliyo na uongozi mzuri. Lakini Mungu hafikirii hivyo. Anaamini kuwa nchi ambapo hakuna mtu anayemwabudu ndiyo Atakayoangamiza. Njia ya mwanadamu ya kufikiria ni tofauti kabisa na ya Mungu. Kwa hivyo, kama mkuu wa nchi hamwabudu Mungu, basi majaliwa ya nchi hii itakuwa ya kutisha, na nchi haitakuwa na majaliwa.

Mungu hashiriki katika siasa za mwanadamu, lakini majaliwa ya nchi ama taifa

inadhibitiwa na Mungu, Mungu anadhibiti dunia hii na ulimwengu mzima. Majaliwa ya mwanadamu na mpango wa Mungu yanashikamana kwa undani, na hakuna mwanadamu, nchi ama taifa limetolewa kwa mamlaka ya Mungu. Iwapo mwanadamu anatamani kujua majaliwa yake, basi lazima aje mbele ya Mungu. Mungu atawafanya wanaomfuata na kumwabudu kufanikiwa, na Atashusha na kuwaangamiza wale wanaompinga na kumkataa.

Kumbuka tukio katika Biblia ambapo Mungu aliangamiza Sodoma, na fikiria pia jinsi mke wa Lutu alivyokuwa nguzo ya chumvi. Fikiria nyuma jinsi watu wa Ninawi walitubu dhambi zao kwa gunia na majivu, na kumbuka kilichofuata baada ya Wayahudi kumsulubisha Yesu miaka 2,000 iliyopita. Wayahudi walitolewa Israeli na kukimbilia nchi duniani kote. Wengi waliuwawa, na taifa lote la Kiyahudi lilikabiliwa na uharibifu wa kipekee. Walimsulubisha Mungu—wakafanya uhalifu wa kuchukiza—na kuchochea tabia ya Mungu. Walifanywa kulipa kwa ajili ya walichofanya, walifanywa kukubali matokeo ya vitendo vyao. Walimlaani Mungu, walimkataa Mungu, na hivyo walikuwa na majaliwa moja pekee: kuadhibiwa na Mungu. Haya ndiyo matokeo machungu na maafa ambayo viongozi wao waliletea nchi na taifa lao.

Leo, Mungu amerudi duniani kufanya kazi Yake. Atasimama kwanza kwa mkutano mkubwa wa viongozi madikteta: Uchina, ngome kali ya ukanaji Mungu. Mungu amepata kundi la watu kwa hekima na nguvu Zake. Wakati huu, Anawindwa na chama tawala cha Uchina kwa kila namna na kukabiliwa na mateso makubwa, bila mahala pa kupumzisha kichwa Chake na kutoweza kupata makazi. Licha ya haya, Mungu bado anaendelea kufanya kazi Aliyonuia kufanya: Anatamka sauti Yake na kueneza injili. Hakuna anayeweza kuelewa uweza wa Mungu. Uchina, nchi inayomchukulia Mungu kama adui, Mungu hajawahi kukoma kazi Yake. Badala yake, watu zaidi wamekubali kazi na neno Lake, kwani Mungu anafanya yote Awezayo kuokoa kila mshiriki wa ubinadamu. Tunaamini hakuna nchi ama nguvu inayoweza kuzuia yale anayotaka kutimiza Mungu. Wale wanaozuia kazi ya Mungu, wanaopinga neno la Mungu, kuvuruga na kudhoofisha mpango wa Mungu hatimaye wataadhibiwa na Mungu. Anayeasi kazi ya Mungu atatumwa kuzimu; nchi yoyote inayoasi kazi ya Mungu itaangamizwa; taifa lolote linaloinuka kupinga kazi ya Mungu litafutwa kutoka dunia hii, na litakoma kuwepo. Nahimiza watu wa mataifa, nchi na hata viwanda vyote kusikiza sauti ya Mungu, kutazama kazi ya Mungu, kuzingatia majaliwa ya mwanadamu, hivyo kumfanya Mungu kuwa mtakatifu zaidi, wa heshima zaidi, wa juu zaidi na chombo cha pekee cha kuabudu miongoni mwa wanadamu, na kuruhusu wanadamu wote kuishi chini ya baraka za Mungu, kama tu ukoo wa Ibrahimu ulivyoishi chini ya ahadi ya Yehova, na kama tu Adamu na Hawa, walioumbwa awali na Mungu, walivyoishi kwa Bustani ya Edeni.

Kazi ya Mungu ni kama mawimbi yanayotapakaa kwa nguvu. Hakuna anayeweza kumweka

kizuizini, na hakuna anayeweza kusimamisha nyayo Zake. Wale tu wanaosikiza maneno Yake kwa makini, na wanaomtafuta na kuwa na kiu naye, wanaweza kufuata nyayo Zake na kupokea ahadi Zake. Wasiofanya hivyo watakabiliwa na maafa makuu na adhabu inayostahili.

Mwanadamu Anaweza tu Kuokolewa Katikati ya Usimamizi wa Mungu

Kila mtu anahisi kuwa usimamizi wa Mungu ni wa ajabu, kwa sababu watu wanafikiri kuwa usimamizi wa Mungu hauna uhusiano wowote na mwanadamu. Wanafikiri kuwa usimamizi wa Mungu ni kazi ya Mungu pekee, shughuli za Mungu, na hivyo wanadamu hawajali kuhusu usimamizi wa Mungu. Kwa njia hii, kuokolewa kwa wanadamu kumekuwa kusiko yakini na kusiko dhahiri, na kumbaki tu maneno matupu. Hata kama mwanadamu anamfuata Mungu ili aokolewe na aingie katika hatima inayopendeza, mwanadamu hajishughulishi na jinsi ambavyo Mungu Hutekeleza kazi Yake. Mwanadamu hashughulishwi na Anachokipanga Mungu na anachopaswa kufanya ili aokolewe. Huzuni iliyoje! Kuokolewa kwa mwanadamu hakuwezi kutenganishwa na usimamizi wa Mungu, aidha hakuwezi kutenganishwa na mipango ya Mungu. Na bado mwanadamu hafikirii chochote kuhusu usimamizi wa Mungu, na hivyo anaendelea kujitenga mbali na Yeye. Hili limesababisha ongezeko la idadi ya watu ambao hawajui kabisa masuala yanayohusiana kwa karibu na suala la wokovu—kama vile uumbaji ni nini, kuamini kwa Mungu ni nini, jinsi ya kumwabudu Mungu, na kadhalika. Kufikia sasa, basi, lazima tuzungumze kuhusu usimamizi wa Mungu, ndiposa kila mfuasi ajue wazi umuhimu wa kumfuata Mungu na kumwamini. Watakuwa na uwezo wa kuchagua njia watakayoifuata ipasavyo, badala ya kumfuata Mungu tu ili kupata baraka, au kuepukana na majanga, au kuwa na mafanikio.

Japo usimamizi wa Mungu waweza kuonekana mkubwa kwa mwanadamu, si jambo la kutofahamika kwa mwanadamu, kwa kuwa kazi yote ya Mungu imefungamanishwa na usimamizi wake, inahusiana na Kazi ya kuokoa mwanadamu, na inajishughulisha na maisha, kuishi, na hatima ya wanadamu. Kazi ambayo Mungu Anaifanya kati ya na kwa mwanadamu, yaweza kusemwa kuwa, ni ya utendaji na yenye maana kubwa. Inaweza kuonekana na mwanadamu, kuhusishwa na mwanadamu, na iko mbali na dhahania. Kama mwanadamu hana uwezo wa kukubali kazi zote Anazozifanya Mungu, basi ni upi umuhimu wa kazi hii? Na ni vipi usimamizi huu unaweza kusababisha kuokolewa kwa mwanadamu? Wengi wa watu wanaomfuata Mungu wanashughulika tu na jinsi watakavyopata baraka nyingi na kuepuka majanga. Panapotajwa kazi na usimamizi wa Mungu, wanakaa kimya na kupoteza matamano yao yote. Wanaamini kuwa kujua maswali ya kuchosha kama hayo hakutakuza maisha yao au kuwa na faida yoyote, na kwa hivyo hata kama wamezisikia habari kuhusu usimamizi wa Mungu, wanazichukulia kikawaida. Na hawazichukulii kama kitu cha thamani kukipokea, na

hata kukikubali kama sehemu ya maisha yao. Watu kama hao wana nia sahili sana katika kumfuata Mungu, na nia hiyo ni kupokea Baraka. Watu kama hao hawawezi kujishughulisha kuzingatia kitu chochote kingine ambacho hakihusiani na nia hii moja kwa moja. Kwao, kuamini kwa Mungu ili kupata baraka ndilo lengo halali na la thamani kwa imani yao. Hawaathiriwi na kitu chochote ambacho hakiwezi kutekeleza lengo hili. Hivyo ndivyo ilivyo na watu wengi wanaomfuata Mungu leo. Nia yao na motisha huonekana kuwa halali, kwa sababu wakati huo huo wa kumwamini Mungu, wanatumia rasilimali kwa ajili ya Mungu, wanajitolea kwa Mungu, na kutekeleza wajibu wao. Wanauacha ujana wao, wanajinyima kwa familia na kazi zao, na hata hukaa miaka mingi wakijishughulisha mbali na nyumbani kwao. Kwa ajili ya lengo lao kuu, wanabadili matamania yao, wanabadili mtazamo wao wa nje wa maisha, hata kubadili njia wanayoitafuta, ila bado hawawezi kubadili nia ya imani yao kwa Mungu. Wanajishughulisha na usimamizi wa matamania yao wenyewe; haijalishi njia iko mbali vipi, na ugumu na vikwazo vilivyo njiani, wanashikilia msimamo wao bila uoga hadi kifo. Ni nguvu zipi zinazowafanya wawe wa kujitolea kwa njia hii? Ni dhamiri yao? Ni sifa zao kubwa na nzuri? Ni kujitolea kwao kupigana na nguvu za maovu hadi mwisho? Ni imani yao wanayomshuhudia Mungu kwayo bila kutaka malipo? Ni utiifu wao ambao kwao wanajitolea kuacha kila kitu ili kutimiza mapenzi ya Mungu? Au ni roho yao ya kujitolea ambayo kwayo wanajinyima kila mara mahitaji badhirifu ya kibinafsi? Kwa watu ambao hawajawahi kujua kazi ya usimamizi wa Mungu kutoa zaidi, kwa hakika, ni muujiza wa ajabu! Hivi sasa, acha tusijadiliane kuhusu kiasi ambacho hawa watu wametoa. Tabia yao, hata hivyo, inastahili sana sisi kuichambua. Mbali na manufaa ambayo yanahusiana nao, je, kuna uwezekano wa kuweko kwa sababu nyingine ya wale hawajawahi kumfahamu Mungu kujitolea zaidi Kwake? Kwa hili, tunagundua tatizo ambalo halikutambuliwa hapo awali: Uhusiano wa mwanadamu na Mungu ni ule wa mahitaji ya kibinafsi yaliyo wazi. Ni uhusiano baina ya mpokeaji na mpaji wa baraka. Kwa kuiweka wazi, ni kama ule uhusiano baina ya mwajiriwa na mwajiri. Mwajiriwa hufanya kazi ili tu kupokea malipo yanayotolewa na mwajiri. Katika uhusiano kama huu, hakuna upendo, ila maafikiano tu, hakuna kupenda au kupendwa, ni fadhila na huruma tu; hakuna maelewano, ila hasira iliyofichwa na udanganyifu; hakuna mapenzi, ila ufa usioweza kuzibika. Mambo yanapofikia hapa, nani anaweza kubadilisha mwelekeo kama huu? Na ni watu wangapi ambao wanaweza kufahamu kwa kweli jinsi uhusiano huu ulivyokosa matumaini? Naamini kuwa watu wanapojitosa wenyewe kwenye raha ya kubarikiwa, hakuna anayeweza kukisia jinsi uhusiano na Mungu ulivyo wa aibu na usiopendeza.

Jambo la kusikitisha mno kuhusu imani ya wanadamu kwa Mungu ni kuwa wanadamu wanatekeleza usimamizi wao wenyewe katikati ya kazi ya Mungu na hawasilizi usimamizi wa Mungu. Udhaifu mkubwa wa mwanadamu unaegemea katika jinsi, wakati huo huo anatafuta kujitoa kwa Mungu na kumwabudu, mwanadamu anaunda hatima yake kamilifu na kuhesabu

jinsi ya kupokea baraka kubwa zaidi na hatima iliyo bora zaidi. Hata kama watu watafahamu jinsi walivyo wa kuhurumiwa, wenye chuki na walivyo ovyo, ni wangapi hapo ambao wanaweza kuachana na ukamilifu na matumaini yao? Na ni nani anayeweza kusimamisha hatua zake na kuacha kujifikiria yeye mwenyewe? Mungu Anawahitaji wale watakaojihusisha kwa karibu Naye kukamilisha usimamizi Wake. Anawahitaji wale ambao watatoa mawazo yao na mwili kwa ajili ya kazi Yake ya usimamizi ili kujitoa Kwake; Hawahitaji wale watakaoinua mikono yao na kuomba kutoka Kwake kila siku, na hata wale wanaotoa kidogo na kusubiri kulipwa kwa hilo tendo la kutoa. Mungu Anawadharau wale wanaotoa michango kidogo na kuridhika. Anawachukia wenye roho katili ambao hukataa kazi ya usimamizi Wake na hutaka tu kuongea kuhusu kwenda mbinguni na kupata baraka. Anachukia hata zaidi na wale ambao hufaidika na fursa inayowezeshwa na kazi Anayoifanya katika kuokoa wanadamu. Hii ni kwa sababu hawa watu hawajawahi kushughulishwa na Anachotarajia kupata Mungu kutokana na kazi Yake ya usimamizi. Wanashughulishwa tu na jinsi wanavyoweza kutumia hiyo fursa iliyowezeshwa na kazi ya Mungu ili kupata baraka. Hawajali roho Yake Mungu, kwa kuwa wanajishughulisha na mustakabali na hatima yao. Wale ambao wanakataa kazi ya usimamizi wa Mungu na hawana hata tamanio dogo katika jinsi Mungu Anavyowaokoa wanadamu na mapenzi Yake, wote wanafanya wapendavyo kando na kazi ya usimamizi wa Mungu. Tabia yao haikumbukwi na Mungu, na haikubaliwi na Mungu, na hata haiangaliwi kwa fadhila ya Mungu.

Katika upana wa ulimwengu na anga, viumbe wasiohesabika wanaishi na kuzaana, hufuata sheria ya mzunguko wa maisha na kufuata sheria isiyobadilika. Wanaokufa huenda na hadithi za walio hai, na walio hai hurudia historia hii yenye huzuni ya wale waliokufa. Na kwa hivyo wanadamu hawawezi kujizuia ila kujiuliza wenyewe; Kwa nini tunaishi? Na kwa nini inatulazimu kufa? Nani anayeitawala dunia hii? Na ni nani muumbaji wa mwanadamu? Je, kweli wanadamu waliumbwa na mazingira asilia? Je, kweli wanadamu wana uamuzi juu ya hatima yao? ... Kwa maelfu ya miaka wanadamu wameyauliza haya maswali, tena na tena. Kwa bahati mbaya, jinsi wanadamu wanavyopagawa na haya maswali, ndivyo kiu yao ya sayansi huendelea kukua. Sayansi hupatiana kutosheleza kwa muda na raha ya muda ya mwili, ila haitoshi kumpa mwanadamu uhuru kutokana na upweke, ukiwa, na hofu isiyodhihirika na kutosaidika ndani ya moyo wake. Wanadamu hutumia ujuzi wa kisayansi ambao wanaweza kuona kwa macho na kuelewa kwa akili yake ili kuutuliza moyo wao. Ihali maarifa kama hayo ya kisayansi hayatoshi kuwazuia wanadamu kutafiti siri. Wanadamu hawajui kabisa Mkuu wa ulimwengu na vitu vyote ni nani, sembuse kujua mwanzo na mustakabali wa wanadamu. Wanadamu wanaishi tu, bila budi, katikati ya hii sheria. Hakuna anayeweza kuiepuka wala kuibadilisha kwani katika vitu vyote na katika mbingu kuna Mmoja kutoka milele hadi milele ambaye ni Mkuu wa kila kitu. Ni Yeye ambaye Hajawahi kuonekana na mwanadamu, ambaye wanadamu hawajawahi kumjua,

ambaye wanadamu hawajawahi kuamini kuwepo Kwake, na bado ni Yeye Aliyewapulizia pumzi mababu wa wanadamu na kuwapa wanadamu uhai. Ni Yeye ndiye Huruzuku na kustawisha wanadamu kwa kuishi kwao, na huwaongoza wanadamu hadi siku ya leo. Aidha, Yeye na Yeye pekee ni wa kutegemewa na wanadamu ili kuendelea kuishi. Ni Mkuu wa kila kitu na Hutawala viumbe vyote vyenye uhai chini ya dunia. Huamrisha misimu yote minne, na ni Yeye huita upepo, jalidi, theluji na mvua. Huwapa wanadamu mwangaza wa jua na huleta machweo ya jioni. Ni Yeye Aliyeumba mbingu na ardhi, Akampa mwanadamu milima, maziwa na mito na kila kitu kilicho na uhai ndani yake. Matendo Yake yamo kila mahali, nguvu Zake ziko kila mahali, busara Zake ziko kila mahali na mamlaka Yake yako kila mahali. Kila mojawapo ya hizi sheria na kanuni ni mfano mzuri wa matendo Yake, na kila mojawapo inafichua hekima na mamlaka Yake. Nani anayeweza kujiondoa kutoka kwa ukuu Wake? Na ni nani anayeweza kujitoa mwenyewe katika njia Zake? Kila kitu kinaishi chini ya uangalizi Wake, zaidi ya hayo, kila kitu huishi chini ya ukuu Wake. Matendo na nguvu Zake huwaacha wanadamu bila chaguo ila kutambua ukweli kwamba ni Yeye pekee Anayeishi na Ana ukuu juu ya kila kitu. Hakuna kitu chochote ila Yeye kinachoweza kuamuru dunia, wala kuwajibikia wanadamu bila kukoma. Bila kujali kama unaweza kutambua vitendo vya Mungu, bila kujali kama unaamini katika kuwepo kwa Mungu, hakuna shaka kuwa hatima yako inaegemea katika mipango ya Mungu, na hakuna shaka kuwa Mungu atakuwa na ukuu juu ya kila kitu. Uwepo na utawala Wake haviwezi kutabiriwa ikiwa vinatambulika na kufahamika na binadamu au la. Ni Yeye pekee Anayejua kuhusu yaliyopita ya mwanadamu, yaliyomo na yanayojiri, na Yeye pekee ndiye mwamuzi wa hatima ya wanadamu. Haijalishi kama unaukubali huu ukweli, haitachukua muda mrefu kabla mwanadamu kushuhudia haya yote kwa macho yake mwenyewe, na huu ni ukweli ambao hivi karibu Mungu Ataudhihirisha. Wanadamu huishi na hufa chini ya macho yake Mungu. Wanadamu huishi kwa usimamizi wa Mungu, na wakati macho Yake yatafumbika kwa mara ya mwisho, hio pia ni kwa usimamizi Wake. Tena na tena, mwanadamu huja na kwenda, nyuma na mbele. Bila mapendeleo, yote ni sehemu ya ukuu na michoro ya Mungu. Usimamizi wa Mungu ungali unaendelea mbele na haujawahi kusimama. Atawafanya wanadamu wafahamu uwepo Wake, waamini katika ukuu Wake, watazame matendo Yake, na warudi katika ufalme Wake. Huu ni mpango Wake, na kazi ambayo Amekuwa Akiitekeleza kwa maelfu ya miaka.

Kazi ya usimamizi wa Mungu ilianza Alipoumba ulimwengu, na mwanadamu ni kiini cha kazi Yake. Uumbaji wa Mungu wa kila kitu, unaweza kusemwa, ni kwa ajili ya mwanadamu. Kwa sababu Kazi ya usimamizi Wake imesambaa katika maelfu ya miaka, na haijatekelezwa katika dakika na sekunde tu, ama kufumba na kufumbua, ama katika mwaka mmoja au miwili, ilimbidi Aumbe vitu vingine zaidi kwa ajili ya maisha ya mwanadamu, kama vile jua, mwezi, na aina zote za viumbe walio hai, na chakula na mazingira kwa ajili ya wanadamu. Huu ndio

ulikuwa mwanzo wa usimamizi wa Mungu.

Baada ya hapo, Mungu Alimkabidhi mwanadamu kwa Shetani, mwanadamu aliishi chini ya miliki ya Shetani, na hili taratibu lilisababisha kazi ya Mungu ya enzi ya kwanza: hadithi ya Enzi ya Sheria.... Kipindi cha miaka elfu kadhaa za Enzi ya Sheria, wanadamu walikuwa wazoefu wa maelekezo ya Enzi ya Sheria, na wakaanza kupuuza, na taratibu wakaacha ulinzi wa Mungu. Na hivyo, pamoja na kushikilia sheria, walimwabudu Mungu na kutenda matendo maovu. Walikuwa bila ulinzi wa Yehova, na waliishi tu mbele ya madhabahu ndani ya hekalu. Kwa kweli, Kazi ya Mungu ilikuwa imejitenga nao kitambo sana, na hata kama Waisraeli walijikita katika sheria, na kulitaja jina la Yehova, na kwa majivuno kuamini kuwa wao pekee ndio walikuwa watu wa Yehova na walikuwa wamechaguliwa na Yehova, utukufu wa Mungu uliwaacha kimyakimya ...

Mungu Anapofanya kazi Yake, huacha sehemu moja na taratibu hutekeleza kazi Yake katika sehemu nyingine mpya. Hii huonekana ya kiajabu sana kwa watu ambao wamepooza. Watu wameishi kuvithamini vya zamani na kuvirejelea vipya, vitu visivyofahamika kwa uhasama, au hata kuonekana kama bughudha. Aidha, kazi yoyote mpya Aifanyayo Mungu, kutoka mwanzo hadi mwisho, mwanadamu ndiye huwa wa mwisho kufahamu kuihusu miongoni mwa kila kitu.

Kama ilivyokuwa kawaida, baada ya kazi ya Yehova katika Enzi ya Sheria, Mungu Alianza kazi yake ya hatua ya pili: kwa kuutwaa mwili—kuwa na mwili kama binadamu kwa miaka kumi, ishirini—na kuongea na kufanya kazi Yake Kati ya waumini. Na bado bila mapendeleo, hakuna aliyejua, na ni idadi ndogo tu ya watu walitambua kuwa Alikuwa Mungu Aliyepata mwili baada ya Yesu Kristo kupigiliwa misumari msalabani na kufufuka. Kwa taabu, palitokea mmoja aliyeitwa Paulo, aliyejitolea kuwa adui wa kuua watu wa Mungu. Hata baada ya kuangushwa chini na kuwa mtume, hali yake ya zamani haikubadilika, na alitembea njia ya kumpinga Mungu. Wakati alipofanya kazi, Paulo aliandika barua nyingi; kwa bahati mbaya, vizazi vya baadaye vilifurahia barua zake kama maneno ya Mungu, kiasi kwamba ziliwekwa ndani ya Agano Jipya na kutatizana na maneno yaliyosemwa na Mungu. Hii kwa kweli ni aibu kubwa tangu majilio ya Maandiko Matakatifu! Na je, hili kosa halikutendwa na mwanadamu kutokana na upumbavu wake? Hawakujua kuwa, katika rekodi za kazi ya Mungu katika Enzi ya Neema, barua na maandiko matakatifu ya mwanadamu hayafai kuwa hapo kuiga kazi na maneno ya Mungu. Lakini hii ni kando na hoja, acha turejeele mada ya awali. Baada tu ya kazi ya Mungu katika hatua ya pili kukamilika—baada ya kusulubishwa—kazi ya Mungu ya kutoa mwanadamu kwenye dhambi (ambayo ni kusema, kumtoa mwanadamu mikononi mwa Shetani) ilitimilika. Na hivyo, kutoka wakati huo kuendelea mbele, wanadamu walipaswa tu kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi ili dhambi zao ziweze kusamehewa. Yaani, dhambi za wanadamu hazikuwa tena

kizuizi cha kuufikia wokovu wake na kuja mbele za Mungu na hazikuwa tena nguvu za kushawishi ambazo Shetani alitumia kumlaumu mwanadamu. Hii ni kwa sababu Mungu Mwenyewe Alikuwa Amefanya kazi halisi, na kuwa katika mfano na limbuko la mwili wenye dhambi, na Mungu mwenyewe Alikuwa sadaka ya dhambi. Kwa njia hii, mwanadamu alishuka kutoka msalabani, akiwa amekombolewa na mwili wa Mungu, mfano wa huu mwili wa dhambi. Na hivyo, baada ya kushikwa mateka na Shetani, mwanadamu alikuja hatua moja mbele karibu na kukubali wokovu mbele za Mungu. Kwa hakika, huu ulingo wa kazi ndio ulikuwa usimamizi wa Mungu ambao ulikuwa hatua moja mbali na Enzi ya sheria, na wa kiwango cha ndani kuliko Enzi ya Sheria.

Huu ni mfano wa usimamizi wa Mungu: kuwakabidhi wanadamu kwa Shetani—wanadamu ambao hawajui kile Mungu Alichu, Muumba ni nini, jinsi ya kumwabudu Mungu, na ni kwa nini inafaa kujitoa kwa Mungu—na kutoa utawala huru kwa uovu wa Shetani. Hatua baada ya hatua, Mungu Anamtoa mwanadamu mikononi mwa Shetani, hadi mwanadamu amwabudu Mungu kikamilifu na kumkataa Shetani. Huu ndio usimamizi wa Mungu. Hili linasikika kama hadithi ya visasili; na inaonekana inatatanisha. Watu wanahisi kwamba ni kama hadithi ya visasili, na hii ni kwa sababu hawana fununu kuhusu yaliyomtokea mwanadamu katika maelfu ya miaka iliyopita, sembuse kujua hadithi ngapi ambazo zimetokea katika ulimwengu na anga. Na zaidi ya hayo, hii ni kwa sababu hawawezi kufahamu kinachostaajabisha sana, dunia inayoibua hofu zaidi ambayo iko zaidi ya dunia yakinifu, lakini ambayo macho yao ya mwili yanawazuia kuiona. Inasikika ya kutofahamika kwa mwanadamu. Na hii ni kwa sababu mwanadamu hana ufahamu wa umuhimu wa Mungu kumwoko na umuhimu wa kazi ya usimamizi wa Mungu, na hafahamu jinsi Mungu Anavyotamani zaidi wanadamu wawe. Je, ni wanadamu mfano wa Adamu na Hawa, wasiopotoshwa na Shetani? Hapana! Usimamizi wa Mungu ni kwa ajili ya kupata kikundi cha watu ambao humwabudu Mungu na kujitoa kwake. Hawa wanadamu wamepotoshwa na Shetani, lakini hawamwoni Shetani kama baba yao: hutambua uso usiopendeza wa Shetani, na kuukataa, na kuja mbele Zake Mungu na kukubali hukumu na kuadibu Kwake. Hujua kisichopendeza na jinsi kinavyotofautiana na kile kilicho kitakatifu, na hutambua ukubwa wa Mungu na uovu wa Shetani. Wanadamu kama hawa hawatamfanyia Shetani kazi tena, au kumwabudu Shetani, au kumsetiri Shetani. Hii ni kwa sababu wao ni kikundi cha watu ambao wamemilikiwa na Mungu. Huu ndio umuhimu wa Mungu kuwasimamia wanadamu. Katika kazi ya usimamizi wa Mungu wa wakati huu, wanadamu ndio chombo cha maovu ya Shetani, na kwa wakati uo huo ni chombo cha ukombozi wa Mungu, aidha ni sababu ya vita dhidi ya Mungu na Shetani. Wakati sawia na wakati wa kutekeleza kazi Yake, Mungu taratibu Humtoa mwanadamu kutoka mikononi mwa Shetani, na hivyo mwanadamu anakuja karibu zaidi na Mungu ...

Baadaye kukaja Enzi ya Ufalme, ambayo ni hatua ya utendaji zaidi na bado ni ngumu zaidi

kukubalika na mwanadamu. Hii ni kwa sababu jinsi mwanadamu ajavyo karibu na Mungu, ndivyo afikapo karibu na kiboko cha Mungu, na ndivyo uso wa Mungu unavyokuwa wazi mbele ya mwanadamu. Kwa kufuatia kukombolewa kwa wanadamu, mwanadamu kirasmi anarejelea familia ya Mungu. Mwanadamu alifikiria kuwa huu ndio wakati wa kufurahia, bado ameegemezwa kwa shambulizi la Mungu na mifano ya yale ambayo bado hayajaonekana na yeyote: Inavyokuwa, huu ni ubatizo ambao watu wa Mungu wanapaswa “kuufurahia.” Katika muktadha huo, watu hawana lingine ila kuacha na kujifikiria wao wenyewe, Mimi ndimi mwanakondoo, aliyepotea kwa miaka mingi, ambaye Mungu Amegharamika kumnunua, sasa kwa nini Mungu Ananitendea hivi? Ama ni njia ya Mungu kunicheka, na kunifichua? ... Baada ya miaka mingi kupita, mwanadamu amedhoofika, kwa kuupitia ugumu wa usafishaji na kuadibu. Ijapokuwa mwanadamu amepoteza “utukufu” na “mapenzi” ya wakati uliopita, bila ya kufahamu amekuja kuelewa kanuni za tabia ya mwanadamu, na amekuja kutambua kazi ya Mungu ya kujitolea kuokoa wanadamu. Taratibu mwanadamu anaanza kuchukia ushenzi wake mwenyewe. Anaanza kuchukia jinsi alivyo mkali, na lawama kuelekea kwa Mungu, na mahitaji yote yasiyokuwa na mwelekeo aliyodai kutoka Kwake. Wakati hauwezi ukarudishwa nyuma, matendo ya zamani huwa ya kujuta katika kumbukumbu za mwanadamu, na maneno na upendo wa Mungu vinakuwa ndivyo vinavyomwendesha mwanadamu katika maisha Yake mapya. Majeraha ya mwanadamu hupona siku baada ya siku, nguvu humrudia, na akasimama na kutazamia uso Wake mwenye Uweza ... ndipo anagundua kuwa daima Ameishi kando yangu, na kwamba tabasamu Lake na sura Yake ya kupendeza bado zinasisimua. Moyo Wake bado unawajali wanadamu Aliowaumba, na mikono Yake bado ina joto na nguvu kama ilivyokuwa hapo mwanzoni. Ni kama mwanadamu alirudi kwenye bustani ya Edeni, lakini wakati huu mwanadamu hasikizi ushawishi wa nyoka, na hatazami kando na uso wa Yehova. Mwanadamu anapiga magoti mbele ya Mungu, na kutazama uso Wake wenye tabasamu, na kumtolea Mungu kafara yenye thamani—Ee! Bwana wangu, Mungu wangu!

Upendo na huruma za Mungu hupenyeza katika kila sehemu ya kazi ya usimamizi Wake, na bila kujali kama watu wanaweza kuelewa nia njema za Mungu, bado Anafanya Kazi bila kuchoka na Anapania kuikamilisha. Haijalishi ni kwa kiasi gani watu wanaelewa usimamizi wa Mungu, manufaa na usaidizi wa Kazi inayofanywa na Mungu unaweza kukubalika na kila mtu. Labda, leo, hujahisi upendo wowote au maisha yaliyowezeshwa na Mungu, lakini bora tu humwachi Mungu, na hupotezi matumaini yako ya kutafuta ukweli, basi kutakuwa na siku ambapo tabasamu la Mungu litafichuliwa kwako. Kwa kuwa dhumuni la kazi ya usimamizi wa Mungu ni kuwatoa wanadamu wanaomilikiwa na Shetani, sio kuwaacha wanadamu waliopotoshwa na Shetani na kumpinga Mungu.

Septemba 23, 2005

**Maneno ya Kristo Alipokuwa Akitembea Makanisani
(Kiendelezo)**

(Oktoba 17, 2013 hadi Agosti 18, 2014)

**Kumjua Mungu Ndiyo Njia ya Kumcha Mungu na Kuepuka
Maovu**

Kila mmoja anapaswa kuchunguza maisha yake upya ya kumwamini Mungu ili kuona iwapo, katika mchakato wa kumfuata Mungu, ameelewa kwa dhati, amefahamu kwa dhati, na kuja kumjua Mungu kwa dhati, iwapo anajua kweli ni mawazo gani Mungu Anayo kwa aina tofauti za binadamu, na iwapo kweli anaelewa kile ambacho Mungu Anafanya juu yake na jinsi Mungu Anaeleza kila tendo lake. Huyu Mungu, Ambaye yuko kando yako, Akiongoza mwelekeo wa kuendelea kwako, Akiamuru hatima yako, na kukupa mahitaji yako—ni kiasi gani ambacho, katika uchambuzi wako, unaelewa nani kiasi gani ambacho kweli unajua kumhusu Yeye? Je, unajua Anachofanyia kazi kwako kila siku? Je, unajua kanuni na makusudi Anayozingatia katika matendo Yake yote? Unajua jinsi Anavyokuongoza? Unajua mbinu Anazotumia kukupa mahitaji yako? Unajua mbinu ambazo Anatumia kukuongoza? Je, unajua kile Anachotaka kupata kutoka kwako na kile Anachotaka kutimiza kwako? Je, unajua mtazamo Anaohukua katika namna nyingi ambazo unatenda? Unajua iwapo wewe ni mtu Anayependwa na Yeye? Unajua chanzo cha furaha, hasira, huzuni na uchangamfu Wake, fikira na dhana zinazohusiana na hayo, na kiini Chake? Unajua, hatimaye, huyu Mungu ni Mungu wa aina gani ambaye unamwamini? Je, maswali haya na mengine ya aina hii kitu ambacho hujawahi kuelewa ama kuwaza kuyahusu? Katika kufuata imani yako kwa Mungu, umewahi, katika ufahamu halisi na kuyatambua maneno ya Mungu, umeondoa hali za kutomwelewa? Je, baada ya kupokea adhabu na kurudi kwa Mungu, umefikia unyenyekevu halisi na kujali kwa kweli? Je, wakati wa kuadibu kwa Mungu na hukumu, umepata kutambua uasi na asili ya kishetani ya mwanadamu na kupata kiasi kidogo cha kuelewa kuhusu utakatifu wa Mungu? Je, chini ya uongozi na kupata nuru kwa maneno ya Mungu, umeanza kuwa na mtazamo mpya wa maisha? Katika majaribu yaliyotumwa na Mungu, umepata kuhisi kutovumilia Kwake makosa ya mwanadamu na pia kile Anachohitaji kutoka kwako na vile Anavyokuokoa? Iwapo hujui kutomwelewa Mungu ni nini, au jinsi ya kumaliza kutoelewa huku, basi mtu anaweza kusema hujawahi kuingia katika ushirika wa kweli na Mungu na hujawahi kumwelewa Mungu, ama angalau mtu anaweza kusema kuwa hujawahi kuwa na nia ya Kumwelewa. Iwapo hujui nidhamu ya Mungu na kuadibu ni nini, basi kwa hakika hujui kujiwasilisha na kujali ni nini, ama angalau hujawahi kujiwasilisha kwa Mungu kwa kweli au kumjali. Iwapo hujawahi kupitia kuadibu kwa Mungu na hukumu, basi kwa kweli

hutajua utakatifu Wake ni nini, na utakuwa hata na ufahamu dhahiri kiasi kidogo kwa mintarafu ya uasi wa mwanadamu ni nini. Iwapo hujawahi kuwa na mtazamo sahihi wa maisha, au lengo sahihi katika maisha, bali bado uko katika hali ya mshangao na kutokuwa na uamuzi kuhusu njia yako ya maisha ya baadaye, hata kwa kiwango cha kusita kuenda mbele, basi ni dhahiri kuwa hujawahi kupokea nuru na uongozi wa Mungu, na mtu anaweza tu kusema kuwa hujawahi kupewa au kujazwa tena na maneno ya Mungu kwa kweli. Iwapo bado hujapitia majaribu ya Mungu, basi ni hakika kuwa bila shaka hutajua kutovumilia kwa Mungu makosa ya mwanadamu ni nini, wala hutaelewa kile ambacho Mungu Anahitaji hatimaye kutoka kwako, ama hata kidogo zaidi, hatimaye, kazi Yake ya kumsimamia na kumwokoia mwanadamu ni nini. Haijalishi ni kwa miaka mingapi mwanadamu ameamini katika Mungu, iwapo hujawahi kupitia ama kutambua chochote katika maneno ya Mungu, basi kwa hakika hatembezi katika njia ya kuelekea wokovu, imani yake katika Mungu kwa hakika haina chochote, maarifa yake kumhusu Mungu pia kwa hakika ni sufuri, na ni hakika kuwa hana ufahamu wowote kuhusu ni nini kumcha Mungu.

Miliki na uwepo wa Mungu, kiini cha Mungu, tabia ya Mungu—yote yamewekwa wazi katika maneno Yake kwa binadamu. Anapopitia maneno ya Mungu, katika mchakato wa kuyatekeleza mwanadamu atapata kuelewa kusudi la maneno Anayonena Mungu, na kuelewa chemichemi na usuli wa maneno ya Mungu, na kuelewa na kufahamu matokeo yaliotarajiwa ya maneno ya Mungu. Kwa binadamu, haya ni mambo yote ambayo mwanadamu lazima ayapitie, ayatambue, na kuyafikia ili kuufikia ukweli na uzima, kutambua nia ya Mungu, kubadilishwa katika tabia yake, na kuweza kutii mamlaka ya Mungu na mipango. Katika wakati huo ambao mwanadamu anapitia, anafahamu, na kuvifikia vitu hivi, atakuwa kupata kumwelewa Mungu polepole, na katika wakati huu atakuwa pia amepata viwango tofauti vya ufahamu kumhusu Yeye. Kuelewa huku na maarifa havitoki katika kitu ambacho mwanadamu amefikiria ama kutengeneza, ila kutoka kwa kile ambacho anafahamu, anapitia, anahisi, na anashuhudia ndani yake mwenyewe. Ni baada tu ya kufahamu, kupitia, kuhisi, na kushuhudia vitu hivi ndipo ufahamu wa mwanadamu kumhusu Mungu utapata ujazo, ni maarifa anayopata katika wakati huu pekee ndio ulio halisi, wa kweli na sahihi, na mchakato huu—wa kupata kuelewa kwa kweli na ufahamu wa Mungu kwa kuelewa, uzoefu, kuhisi, na kushuhudia maneno Yake—sio kingine ila ushirika wa kweli kati ya mwanadamu na Mungu. Katikati ya aina hii ya ushirika, mwanadamu anakuja kuelewa kwa dhati na kufahamu nia za Mungu, anakuja kuelewa kwa dhati na kujua miliki na uwepo wa Mungu, anakuja na kuelewa kujua kwa kweli kiini cha Mungu, anakuja kuelewa na kujua tabia ya Mungu polepole, anafikia uhakika wa kweli kuhusu, na ufafanuzi sahihi wa, ukweli wa mamlaka ya Mungu juu ya vitu vyote vilivyoundwa, na kupata mkondo kamili kwa na ufahamu wa utambulisho wa Mungu na nafasi Yake. Katika aina hii ya ushirika, mwanadamu anabadilika, hatua kwa hatua, mawazo yake kuhusu Mungu, bila

kumwaza pasi na msingi, ama kuipa nafasi tashwishi yake kumhusu Yeye, ama kutomwelewa, ama kumshutumu, ama kupitisha hukumu Kwake, ama kuwa na shaka Naye. Kwa sababu hii, mwanadamu atakuwa na mijadala michache na Mungu, atakuwa na uhasama kiasi kidogo na Mungu, na kutakuwa na matukio machache ambapo atamuasi Mungu. Kwa upande mwingine, kujali kwa mwanadamu na utii kwa Mungu kutakua kwa kiasi kikubwa, na uchaji wake Mungu utakuwa wa kweli zaidi na pia mkubwa zaidi. Katika ya aina hii ya ushirika, mwanadamu hatapata kupewa ukweli pekee na ubatizo wa uzima, bali wakati uo huo pia atapata maarifa ya kweli ya Mungu. Katika aina hii ya ushirika, mwanadamu hatapata kubadilishwa kwa tabia yake na kupata wokovu pekee, bali pia kwa wakati huo atafikia uchaji na ibada ya kweli ya kiumbe aliyeumbwa kwa Mungu. Baada ya kuwa na aina hii ya ushirika, imani ya mwanadamu katika Mungu haitakuwa tena ukurasa tupu wa karatasi, ama ahadi ya maneno matupu, ama harakati na tamani lisilo na lengo na kuabudu kama mungu; katika aina hii ya ushirika pekee ndio maisha ya mwanadamu yatakua kuelekea ukomavu siku baada ya siku, na ni wakati huu ndio tabia yake itabadilika polepole, na imani yake kwa Mungu, hatua kwa hatua, itatoka kwenye imani ya wasiwasi na kutoeleweka na imani isiyo ya hakika mpaka katika utii wa kweli na kujali, na kuwa katika uchaji Mungu wa kweli, na mwanadamu pia, katika mchakato wa kumfuata Mungu, ataendelea polepole kutoka kuwa mtazamaji na kuwa na hali ya utendaji, kutoka yule anayeshughulikwa na kuwa anayechukua nafasi ya kutenda; kwa aina hii ya ushirika pekee ndipo mwanadamu atafikia kuelewa kwa kweli na ufahamu wa Mungu, kwa ufahamu wa kweli wa Mungu. Kwa sababu watu wengi hawajawahi kuiingia katika ushirika wa kweli na Mungu, ufahamu wao wa Mungu unakomea kiwango cha nadharia, katika kiwango cha barua na kanuni. Hivyo ni kusema, watu wengi, haijalishi ni miaka mingapi wamemwamini Mungu, ikija kwa kumjua Mungu bado wako mahali walipoanzia, wamekwama katika msingi wa aina za heshima, na mitego yao ya hadhi na kabaila za kishirikina. Kwamba maarifa ya mwanadamu kumhusu Mungu yanapaswa kukomea yalipoanzia ina maana kwamba hayapo kabisa. Mbali na uthibitisho wa mwanadamu kuhusu nafasi ya Mungu na utambulisho, imani ya mwanadamu kwa Mungu bado iko katika hali ya kutoeleweka na kutokuwa na uhakika. Hii ikiwa hivyo, ni kiasi gani ambacho mwanadamu anaweza kuwa nacho kuhusu uchaji Mungu wa kweli?

Haijalishi kiwango cha imani yako katika uwepo Wake, hili haliwezi kuchukua mahali pa ufahamu wako wa Mungu, wala uchaji wako wa Mungu. Haijalishi kiwango ambacho umefurahia baraka Zake na neema Yake, hii haiwezi kuchukua nafasi ya ufahamu wako wa Mungu. Haijalishi ni kiwango gani unataka kuweka wakfu kila kitu chako na kugharimika kwa ajili Yake, hii haiwezi kuchukua nafasi ya maarifa yako kuhusu Mungu. Ama labda umeyazoea sana maneno ambayo Amenena mpaka unayajua kimoyomoyo na unaweza kuyasema upesi kinyumenyume; hata hivyo, hii haiwezi kuchukua nafasi ya maarifa yako kuhusu Mungu.

Haijalishi kiwango cha dhamira ya mwanadamu katika kumfuata Mungu, iwapo hajawahi kuwa na ushirika wa kweli na Mungu, ama kuwa na uzoefu wa kweli wa maneno ya Mungu, basi ufahamu wake wa Mungu utakuwa utupu tu au ndoto isiyo na mwisho; kwa kuwa yote yale unaweza kuwa “umekumbana” na Mungu kwa kupita, au kukutana Naye uso kwa uso, ufahamu wako wa Mungu bado utakuwa sufuri, na uchaji wako wa Mungu utakuwa tu kidahizo ama njozi.

Watu wengi huyashika maneno ya Mungu kuyasoma siku baada ya siku, kiasi kwamba wanaviweka akilini vifungu vyote maarufu humo kama vitu vyao vyenye thamani zaidi, na zaidi kuyahubiri maneno ya Mungu kila mahali, wakiwatolea na kuwasaidia wengine kwa njia ya maneno Yake. Wanafikiri kuwa kufanya hivi ni kuwa na ushuhuda kwa Mungu, kuwa na ushuhuda kwa maneno Yake, kwamba kufanya hivi ni kufuata njia ya Mungu; wanafikiri kuwa kufanya hivi ni kuishi kulingana na maneno ya Mungu, kwamba kufanya hivi ni kuleta maneno Yake katika maisha yao halisi, kuwa kufanya hivi kutawawezesha kupokea pongezi ya Mungu, na kuokolewa na kukamilika. Lakini, hata wanapohubiri maneno ya Mungu, hawazingatii maneno ya Mungu katika matendo, ama kujaribu kujileta sambamba na yale yanayofichuliwa katika maneno ya Mungu. Badala yake, wanayatumia maneno ya Mungu kupata upendo na imani ya wengine kwa hila, kuingia katika usimamizi wao wenyewe, na kubadhiri na kuiba sifa za Mungu. Wanatarajia, kwa ubatili, kutumia nafasi waliyopata kwa kueneza maneno ya Mungu ili kupewa kazi ya Mungu na pongezi Yake. Miaka mingapi imepita, lakini hao watu hawajaweza tu kupata pongezi ya Mungu katika hatua ya kuyahubiri maneno ya Mungu, na hawajaweza tu kugundua njia ambayo wanafaa kufuata katika hatua ya kushuhudia maneno ya Mungu, na hawajajisaidia tu ama kujipatia wenyewe katika hatua ya kuwapa na kuwasaidia wengine kwa njia ya maneno ya Mungu, na hawajaweza tu kumjua Mungu, ama kuamsha ndani yao uchaji wa kweli wa Mungu, katika hatua ya kufanya haya yote; kwa upande mwingine, kutoelewa kwao kuhusu Mungu kunakuwa hata wenye kina zaidi, kutokuwa na imani kwao kwa Mungu kunazidi kuwa na mashaka, na mawazo yao kumhusu yanatiwa chumvi zaidi. Wakijazwa na kuongozwa na mawazo yao kuhusu maneno ya Mungu, wanaonekana kuwa katika haki yao kamili, kana kwamba wanapitia ujuzi wao bila juhudi, kana kwamba wamepata kusudi lao katika maisha, wito wao, na kana kwamba wameshinda maisha mapya na kuokolewa, kana kwamba, maneno ya Mungu yakibiringika kutoka kwenye ulimi kwa kukariri, wameupata ukweli, kushika nia za Mungu, na kugundua njia ya kumjua Mungu, kana kwamba, katika wakati wa kuhubiri maneno ya Mungu, wanakuja kila wakati uso kwa uso na Mungu, pia, wana “sukumwa” kila wakati mpaka kiwango cha kilio, na kila wakati kuongozwa na “Mungu” katika maneno ya Mungu, wanaonekana kushika bila kukoma wasiwasi Wake wenye ari na nia njema, na wakati uo huo kushika wokovu wa Mungu kwa mwanadamu na usimamizi Wake, kuja kujua kiini

Chake, na kuelewa tabia Yake ya haki. Msingi huu ukizingatiwa, wanaoneka kuamini hata zaidi katika uwepo wa Mungu, kujua zaidi hali ya utukufu Wake, na kuhisi hata kwa kina zaidi ukuu Wake na kuvuka mipaka Kwake. Wakiwa wameinuka katika ufahamu wao wa kijuujuu wa maneno ya Mungu, itaonekana kuwa imani yao imekua, kuamua kwao kupitia mateso kumetiwa nguvu, na maarifa yao kwa Mungu yamekuwa na kina. Ila hawajui kwamba, hadi watakapopitia maneno ya Mungu kwa kweli, maarifa yao yote kuhusu Mungu na mawazo yao kumhusu Yeye yanatoka kwa mawazo yao wenyewe ya kufikiri kwa ubunifu na kukisia. Imani yao haiwezi kusimama jaribio lolote kutoka kwa Mungu, wanachoita kiroho na kimo haviwezi kusimama chini ya majaribu ya Mungu na ukaguzi, uamuzi wao ni ngome tu iliyojengwa juu ya changarawe, na wanachoita maarifa juu ya Mungu pia sio zaidi ya ubunifu wa mawazo yao. Kwa hakika, watu hawa, ambao, ilivyokuwa, wameweka juhudi kubwa katika maneno ya Mungu, hawajawahi kutambua imani ya kweli ni nini, kujiwasilisha kwa kweli ni nini, kujali kwa kweli ni nini, ama maarifa ya kweli ya Mungu ni nini. Wanachukua nadharia, mawazo, maarifa, zawadi, utamaduni, ushirikina na hata tabia nzuri za binadamu, na kuyafanya kuwa “mtaji na silaha” za kumwamini Mungu na ufuataji wao wa Mungu, hata kuyafanya kuwa misingi ya imani yao kwa Mungu na katika kumfuata Yeye. Wakati uo huo, pia wanachukua uwekezaji msingi huu na silaha na kuyafanya kuwa hirizi ya uchawi kwa kumjua Mungu, ya kukutana na kubishana na ukaguzi wa Mungu, majaribu, kuadibu, na hukumu. Mwishowe, wanachopata bado hakijumlishi chochote zaidi ya hitimisho kumhusu Mungu zinazoegemea hisia za kidini, katika kabaila za ushirikina, na kwa yote yaliyo ya kimapenzi, ya kustaajabisha, na yenye ugumu kuelewa, na njia yao ya kujua na kumweleza Mungu imepigwa muhuri katika muundo sawa na wa wale watu wanaoamini katika Mbingu iliyo Juu pekee, ama Mtu Mzee aliye Mawinguni, wakati ukweli wa Mungu, kiini Chake, tabia Zake, miliki Zake na asili, na kadhalika, yote yanayomhusu Mungu wa kweli Mwenyewe, ni vitu ambavyo kuvijua kumekosa mshiko, havina uhusiano kabisa na viko mbali kabisa. Katika njia hii, ingawa wanaishi chini ya upaji na ustawishaji wa maneno ya Mungu, hawawezi hata hivyo kutembea kwa kweli katika njia ya kumcha Mungu na kuepuka maovu. Sababu ya hakika ya hii ni kwamba hawajawahi kupata kujuana na Mungu, wala hawajawahi kuwa na mawasiliano ya kweli ama ushirika Naye, kwa hivyo haiwezekani kufikia maelewano ya pamoja na Mungu, ama kuamsha ndani mwao imani halisi katika, kufuata, ama ibada ya Mungu. Kwamba wanafaa kuyahusisha maneno ya Mungu, kwamba wanafaa kumhusisha Mungu—mwelekeo huu na tabia imewahukumu kurudi mkono mtupu kutoka kwa jitihada zao, imewahukumu katika maisha yote wasiweze kutembea katika njia ya kumcha Mungu na kuepuka maovu. Lengo wanalolengea, na mwelekeo wanaoelekea, inamaanisha kuwa ni maadui wa Mungu milele, na kwamba hata milele hawatawahi kuweza kupokea wokovu.

Iwapo, katika tukio la mwanadamu ambaye amemfuata Mungu kwa miaka mingi na kufurahia kupewa maneno Yake kwa miaka mingi, ufafanuzi wake kuhusu Mungu ni, katika kiini chake, sawa na ule wa mtu anayejisujudu kwa heshima mbele ya sanamu, basi hii itamaanisha kuwa huyu mtu hajakata ukweli wa maneno ya Mungu. Kwa kutazama katika chanzo cha hii, mtu anaona kuwa tu hajaingia katika ukweli wa maneno ya Mungu, na kwa sababu hii hali halisi, ukweli, nia, na matarajio juu ya binadamu, yote ambayo yana asili kwa maneno ya Mungu, hayana uhusiano wowote na yeye. Hivyo ni kusema, haijalishi ni kiwango gani mwanadamu wa aina hii anaweza kufanya bidii katika maana ya juu ya maneno ya Mungu, yote ni bure: kwani yale anayofuata ni maneno tu, kwa hivyo yale atakayopata yatakuwa pia ni maneno tu. Haijalishi kama maneno yanayonenwa na Mungu ni makavu au makubwa katika mwonekano wa nje, yote ni ukweli ulio lazima kwa mwanadamu anapoingia katika uzima; ni chemichemi ya maji ya uzima yanayomwezesha kuishi katika roho na mwili. Yanatosheleza kile ambacho mwanadamu anahitaji ili awe hai; kanuni na imani ya kufanya maisha yake ya kila siku; njia, lengo, na mwelekeo ambao lazima apitie ili kupokea wokovu; kila ukweli ambao anapaswa awe nao kama kiumbe aliyeumbwa mbele za Mungu; na kila ukweli jinsi mwanadamu anavyotii na kumwabudu Mungu. Ni uhakika ambao unahakikisha kuishi kwa mwanadamu, ni mkate wa kila siku wa mwanadamu, na pia ni nguzo ya msaada inayoweza mwanadamu kuwa na nguvu na kusimama. Yamejaa utajiri wa ukweli wa ubinadamu wa kawaida anavyoishi binadamu aliyeumbwa, yamejaa ukweli ambao mwanadamu anatumia kutoka kwa upotovu na kuepuka mitego ya Shetani, yamejaa mafunzo bila kuchoka, kuonya, kuhamasisha na furaha ambayo Muumba anampa binadamu aliyeumbwa. Ni ishara ambayo inawaongoza na kuwaelimisha wanadamu kuelewa yale yote yaliyo mazuri, hakika inayohakikisha kuwa wanadamu wataishi kwa kudhihirisha na kumiliki yale yote yaliyo ya haki na mema, kigezo ambacho watu, matukio, na vitu vyote vinapimwa, na pia alama ya usafiri inayowaongoza wanadamu kuelekea wokovu na njia ya mwanga. Katika uzoefu wa vitendo wa maneno ya Mungu tu ndipo mwanadamu anaweza kupewa ukweli na uzima; humu pekee ndimo anaweza kuja kupata kuelewa ubinadamu wa kawaida ni nini, maisha yenye umuhimu ni nini, kiumbe halisi ni nini, utiifu wa kweli kwa Mungu ni nini; humu pekee ndimo anaweza kuja kuelewa anavyofaa kumjali Mungu, jinsi ya kutimiza wajibu ya kiumbe aliyeumbwa, na jinsi ya kumiliki mfano wa mwanadamu wa kweli; humu tu ndimo anaweza kupata kuelewa maana ya imani halisi na ibada halisi; humu tu ndimo anaweza kuelewa nani ndiye Mtawala wa mbingu na nchi na vitu vyote; humu tu ndimo mwanadamu anaweza kuja kuelewa njia ambayo Yule ambaye ni Bwana wa uumbaji wote Anatawala, anaongoza, na kuutosheleza uumbaji; na hapa pekee ndipo anaweza kuja kuelewa na kushika njia ambayo Yule aliye Bwana wa uumbaji wote Anakuwa, Anadhihirishwa na kufanya kazi. Akitenganishwa na uzoefu wa kweli wa maneno ya Mungu, mwanadamu hana maarifa ya kweli ama ufahamu katika maneno ya Mungu na ukweli.

Mwanadamu wa aina hii ni maiti inayoishi tu, ganda lililoisha, na ufahamu wote unaohusiana na Muumba hauna chochote kingine kumhusu. Katika macho ya Mungu, mwanadamu kama huyo hajawahi kumwamini, ama kuwahi kumfuata, na hivyo Mungu hamtambui yeye kama mwumini Wake wala mfuasi Wake, ama hata kama kiumbe halisi aliyeumbwa.

Ili kuwa kiumbe halisi aliyeumbwa, sharti ujue Muumba ni nani, uumbaji wa mwanadamu ni wa umuhimu gani, jinsi ya kutekeleza majukumu ya kiumbe, na jinsi ya kumwabudu Bwana wa uumbaji wote, lazima aelewe, ashike, ajue, na kujali kuhusu nia za Muumba, mapenzi Yake, na madai Yake, na lazima atende kulingana na njia ya Muumba—kumcha Mungu na kuepuka maovu.

Kumcha Mungu kuna maana gani? Na mtu anawezaje kuepuka maovu?

“Kumcha Mungu” hakumaanishi woga na hofu isiyotajika, wala kukwepa, wala kuweka umbali, wala si kuabudu kama mungu ama ushirikina. Ila, ni kutazama na kupendezwa, sifa, imani, kuelewa, kujali, kutii, kuweka wakfu, upendo, na pia ibada isiyo na vikwazo au malalamishi, malipo na kutii. Bila ya ufahamu halisi wa Mungu, binadamu hawatakuwa na kupendezwa halisi, imani halisi, kuelewa halisi, kujali halisi ama utiifu, ila tu hofu na kukosa utulivu, shaka pekee, kutoelewa, kukwepa, na kuepuka; bila maarifa halisi ya Mungu, binadamu hawatakuwa na utakatifu na malipo halisi; bila ufahamu halisi wa Mungu, binadamu hawatakuwa na ibada halisi na kujisalimisha, uabudu kama mungu upofu tu na ushirikina; bila maarifa halisi juu ya Mungu, binadamu hawawezi kutenda kulingana na njia ya Mungu, ama kumcha Mungu, ama kuepuka maovu. Badala yake, kila tendo na tabia ambayo mwanadamu anashiriki litajaa uasi na kutotii, na kumbukumbu zinazokashifu na hukumu ya usengenyaji kumhusu Yeye, na mienendo miovu inayokwenda kinyume na ukweli na maana ya kweli ya maneno ya Mungu.

Punde wanadamu wanapokuwa na imani ya kweli kwa Mungu, watakuwa wa kweli katika kumfuata Yeye na kumtegemea; kwa imani ya kweli pekee na tegemeo kwa Mungu ndipo binadamu watakuwa na kuelewa kwa kina na ufahamu; pamoja na ufahamu wa kweli wa Mungu inakuja kumjali Kwake kwa kweli; ni kwa kumjali Mungu kwa kweli pekee ndipo binadamu watakuwa na utiifu wa kweli kwa Mungu; na ni kwa utiifu wa Mungu kwa kweli pekee ndipo binadamu watakuwa na uwekaji wakfu wa kweli; na ni kwa uwekaji wakfu wa kweli kwa Mungu pekee ndipo binadamu watakuwa na malipo yasiyo na kiwango na kulalamika; ni kwa imani na msimamo wa kweli, kuelewa na kujali kwa kweli, utiifu wa kweli, utakatifu wa kweli na malipo, ndipo binadamu watakuja kujua kwa kweli tabia na kiini cha Mungu, na kujua utambulisho wa Muumba; Watakapopata kumjua Muumba ndipo binadamu wataamsha ndani yao ibada ya kweli na kujisalimisha; watakapokuwa na ibada ya kweli na kujisalimisha kwa

Muumba tu ndipo binadamu wataweza kwa kweli kuweka kando njia zao za uovu, hivyo ni kusema, kuepuka maovu.

Hii inajumlisha hatua yote ya “kumcha Mungu na kuepuka maovu” na pia ni maudhui katika kumcha Mungu na kuepuka maovu kwa ujumla, na pia njia ambayo ni lazima kupitia ili kufikia kumcha Mungu na kuepuka maovu.

“Kumwogopa Mungu na kuepuka maovu” na kumjua Mungu ni uhusiano usiogawanyishwa na uliunganishwa kwa nyuzi zisizohesabika, na uhusiano kati yao ni dhahiri. Iwapo mtu anataka kupata uwezo wa kuepuka maovu, lazima kwanza amche Mungu kwa kweli; iwapo mtu anataka kupata uwezo wa kumcha Mungu kwa kweli, lazima awe na maarifa ya kweli kuhusu Mungu; Iwapo mtu anataka kupata maarifa ya Mungu, lazima kwanza ayapitie maneno ya Mungu, aingie katika ukweli wa maneno ya Mungu, apitie kuadibu na nidhamu ya Mungu, kuadibu Kwake na hukumu; iwapo mtu anataka kupitia maneno ya Mungu, lazima aje ana kwa ana na maneno ya Mungu, aje ana kwa ana na Mungu, na kumwomba Mungu Ampe fursa ya kupitia maneno ya Mungu katika hali ya aina yote ya mazingira inayowahusisha watu, matukio na vitu; iwapo mtu anataka kuja ana kwa ana na Mungu na maneno ya Mungu, lazima kwanza amiliki moyo wa kweli na mwaminifu, awe tayari kuukubali ukweli, kukubali kupitia mateso, uamuzi na ujasiri wa kuepuka uovu, na azimio la kuwa kiumbe halisi...Kwa njia hii, kuendelea mbele hatua kwa hatua, utamkaribia Mungu zaidi, moyo wako utakuwa safi zaidi, na maisha yako na thamani ya kuwa hai, pamoja na maarifa yako kuhusu Mungu, yatakuwa ya maana zaidi na yatakuwa hata ya kupevuka zaidi. Mpaka siku moja, utahisi kuwa Muumba sio fumbo tena, kwamba Muumba hajawahi kufichwa kutoka kwako, kwamba Muumba hajawahi kuificha sura Yake kutoka kwako, kwamba Muumba hayuko mbali na wewe hata kidogo, kwamba Muumba siye yule unayemtamania katika mawazo yako lakini kwamba huwezi kumfikia na hisia zako, kwamba Anasimama kwa kweli kama mlinzi kulia na kushoto kwako, Akiruzuku maisha yako, na kudhibiti majaliwa yako. Hayuko katika upeo wa mbali, wala hajajificha juu mawinguni. Yuko kando yako, akiwa na mamlaka juu ya kila kitu chako, Yeye ni kila kitu ulicho nacho, na Yeye ni kitu pekee ulicho nacho. Mungu kama huyo Anakukubali umpende kutoka moyoni, umshikilie, umweke karibu, umtamani, uhofu kumpoteza, na kutotaka kumkataa tena, kutomtii tena, ama kumwepuka tena ama kumweka mbali. Kile unachotaka ni kumjali tu, kumtii, kulipia kila kitu Anachokupa, na kujisalimisha katika himaya Yake. Hukatai tena kuongozwa, kupewa, kuangaliwa, na kuwekwa na Yeye, hukatai tena Anachoamuru na kukitawaza kwako. Unachotaka tu ni kumfuata, kutembea kando Yake katika kushoto ama kulia Kwake, kile utakacho ni kumkubali kama maisha yako ya pekee, kumkubali kama Bwana wako mmoja na wa pekee, Mungu wako mmoja na wa pekee.

Agosti 18, 2014

Namna ya Kujua Tabia ya Mungu na Matokeo Ambayo Kazi Yake Itafanikisha

Kwanza, hebu tuimbe wimbo wa kumsifu Mungu: Wimbo wa Ufalme (I) Ufalme Unashuka Duniani.

Kiambata: Umati unanishangilia Mimi, umati wananisifu Mimi; vinywa vyote vinamtaja Mungu mmoja wa kweli. Ufalme unashuka juu ya ulimwengu wa wanadamu.

1. Umati unanishangilia, umati unanisifu; watu wote wanalitaja jina la Mungu mmoja wa kweli, watu wote wanayainua macho yao kuviangalia vitendo Vyangu. Ufalme unashuka duniani mwa wanadamu, nafsi Yangu ni ya fahari na yenye neema. Nani asingesherehekea kwa ajili ya hili? Ni nani asingecheza kwa furaha? Ee Sayuni! Inua bendera yako ya ushindi unisherehekee! Imba wimbo wako wa ushindi ili ulieneze jina Langu takatifu!

2. Viumbe wote duniani kote! Harakisheni kujitakasa ili muweze kufanywa kuwa sadaka Kwangu! Nyota juu mbinguni! Rudini kwenye maeneo yenu kwa haraka ili muonyeshe nguvu Yangu kuu katika anga! Nazisikiliza sauti za watu duniani, wanaomimina upendo na uchaji wao mwingi kwa ajili Yangu katika wimbo! Katika siku hii, huku viumbe wote wakirudishiwa uhai, Nashuka katika dunia ya wanadamu. Katika wakati huu, mambo yalivyo, maua yanachanua kwa wingi, ndege wote wanaimba kwa sauti moja, vitu vyote vinajawa na furaha! Kwa sauti ya saluti ya ufalme, ufalme wa Shetani unaanguka, ukiangamizwa katika mngurumo wa wimbo wa ufalme, usiinuke tena!

3. Nani duniani anathubutu kuinuka na kupinga? Ninaposhuka duniani Naleta kuchoma, Naleta ghadhabu, Naleta maafa ya aina yote. Falme za dunia sasa ni ufalme Wangu! Juu angani, mawingu yanagaagaa na kujongea kama mawimbi; chini ya anga, maziwa na mito yanatapakaa na kutoa muziki wa kusonga kwa furaha. Wanyama wanaopumzika wanaibuka kutoka kwenye matundu yao, na watu wote ambao wamelala wanaamshwa nami. Siku ambayo watu wote wameingojea hatimaye imefika! Wananiimbua nyimbo nzuri sana!

Ni nini mnachofikiria kuhusu kila wakati mnapouimba wimbo huu? (Ukiwa umechangamka; nasisimkwa; nafikiria namna ambavyo utukufu wa ufalme ulivyo mrembo, na mwanadamu na Mungu wataunganishwa daima dawamu.) Je, yupo yeyote aliyefikiria kuhusu umbo ambalo binadamu lazima achukue ili kuweza kuwa na Mungu? Katika kufikiria kwenu, mtu anafaa kuwa vipi ili kuweza kujiunga na Mungu na kufurahia maisha yenye utukufu yanayofuata katika ufalme? (Wanafaa kuwa wamebadilisha tabia.) Wanafaa kuwa

wamebadilisha tabia, lakini kubadilisha hadi kiwango gani? Watakuwa vipi baada ya kubadilishwa tabia? (Watakuwa watakatifu.) Ni nini kipimo cha utakatifu? (Fikira na utiliaji maanani wao wote unalingana na Kristo.) Sasa ni vipi ambavyo hali hii ya kuingiliana inavyojionyesha? (Hawamzuii Mungu, wala kumsaliti Mungu, lakini wanajitolea kuwa wenye utiifu kabisa kwa Mungu na kumcha Mungu katika mioyo yao.) Baadhi ya majibu yenu yako katika njia sawa. Fungueni mioyo yenu, nyinyi nyote, na msemazane kile ambacho mioyo yenu inawaambia. (Watu wanaoishi na Mungu katika ufalme wanaweza kutekeleza wajibu wao, kutekeleza kwa uaminifu wajibu wao, kwa kutafuta ukweli na kutozuiliwa na mtu yeyote, hafla yoyote, au kifaa chochote. Na inawezekana kujiondoa kwenye ushawishi wa giza na kulinganisha mioyo yao na Mungu, na kumcha Mungu na kujiepusha na uovu.) (Mtazamo wetu wa kuangalia mambo unaweza kulinganishwa na ule wa Mungu, na tunaweza kujitenga na ushawishi wa giza. Kiwango cha chini zaidi ni kutotumiwa vibaya na Shetani, kutupa nje tabia yoyote ya upotoshaji, na kutimiza utiifu wa Mungu. Tunasadiki kwamba kuwa huru dhidi ya ushawishi wa giza ndiyo hoja kuu. Kama mtu hawezi kujitenga na ushawishi wa giza, hawezi kujipa uhuru kutoka kwenye minyororo ya Shetani, basi hajakata wokovu wa Mungu.) (Kiwango cha kufanywa kuwa mtimilifu na Mungu ni binadamu akiwa na moyo mmoja na akili na Mungu. Binadamu hamzuii Mungu tena; anaweza kujua Mungu mwenyewe, kuweka ukweli katika matendo, kupata uelewa wa Mungu, kumpenda Mungu, na kulingana na Mungu. Hayo ndiyo yote ambayo mtu anahitaji kufanya.)

Uzito wa Matokeo katika Mioyo ya Watu

Yaonekana mnavyo vitu katika mioyo yenu kuhusu njia mnayofaa kutembea na mmeimarisha mmeimarisha kiwango cha kuielewa au kufahamu. Hata hivyo, iwapo maneno yote ambayo mmeyanena ni maneno matupu au halisi inategemea lengo lenu la matendo yenu ya kila siku. Mmepata mavuno kutoka kwenye dhana zote za ukweli kupitia miaka hii, kwenye falsafa na kwenye maudhui ya ukweli. Hii inathibitisha kwamba watu siku hizi wanatilia mkazo kule kutafuta ukweli. Na kutokana na hayo, kila dhana na kila kipengele cha ukweli kwa hakika kimeweka mizizi kwenye mioyo ya baadhi ya watu. Hata hivyo, ni nini hasa Ninachoogopa sana? Kwamba ingawa wahusika wa ukweli, na nadharia hizi, yameweza kunakili mizizi yao, maudhui halisi bado hayana uzito mkubwa katika mioyo yenu. Wakati mnapokumbana na masuala, mnapopitia majaribio, mnapopitia chaguo—ni kwa kiwango kipi utumiaji wa vitendo wa ukweli huu utakuwa wa manufaa kwenu? Je, inawezekana yatawasaidia kupita ugumu wenu na kuwafanya kuibuka kutoka kwenye majaribio yenu baada ya kutosheleza nia za Mungu? Je, mtasimama imara katika majaribio yenu na kushuhudia kwa sauti na waziwazi kwake Mungu? Je, mmewahi kuwa na kivutio katika masuala haya awali? Mniruhusu kuuliza: Katika mioyo yenu, kwenye fikira na tafakari zenu za kila siku, ni nini hicho ambacho ni muhimu sana kwenu?

Mmewahi kuja kwenye hitimisho? Ni nini mnachosadiki kuwa kitu muhimu zaidi? Baadhi ya watu husema “ni kuweka ukweli katika matendo, bila shaka”; baadhi ya watu husema “bila shaka ni kulisoma neno la Mungu kila siku”; baadhi ya watu husema “ni kujiweka mbele ya Mungu na kuomba Mungu kila siku, bila shaka”; na kisha kunao wale wanaosema “bila shaka ni kutekeleza wajibu wangu kwa njia bora kila siku”; kunao baadhi ya watu pia ambao wanasema wanafikiria wakati wote tu kuhusu namna ya kumtosheleza Mungu, namna ya kumtii Yeye katika mambo yote, na namna ya kuchukua hatua kulingana na mapenzi Yake. Je, hivi ndivyo ilivyo? Je, hivi ndivyo kila kitu kinavyohitajika kufanywa? Kwa mfano, kunao baadhi wanaosema: “Mimi ninataka tu kumtii Mungu, lakini kitu kinapofanyika siwezi kumtii Yeye.” Baadhi ya watu husema: “Nataka tu kumtosheleza Mungu. Hata kama ningemtoshela Yeye mara moja tu, hilo lingetoshwa, lakini sitoweza kumtosheleza Yeye.” Na baadhi ya watu husema: “Ninataka tu kumtii Mungu. Katika nyakati za majaribio nataka kunyenyekea katika mipango Yake, huku nikitii ukuu na mipangilio Yake, bila ya malalamiko au maombi yoyote. Ilhali karibu kila wakati ninashindwa kuwa mtiifu.” Baadhi ya watu wengine husema: “Ninapokabiliwa na uamuzi, siwezi kamwe kutia ukweli katika matendo. Siku zote nataka kutosheleza mwili, siku zote nataka kutosheleza matamania yangu ya kibinafsi ninayojitakia.” Ni nini sababu ya haya? Kabla ya jaribio la Mungu kufika, je, mmewahi kujipa changamoto nyinyi wenyewe mara nyingi, na kujijaribu nyinyi wenyewe mara nyingi? Oneni kama kweli mnaweza kumtii Mungu, kuweza kwa kweli kumtosheleza Mungu, na kuwa na hakika kutomsaliti Mungu. Tazameni kama hamwezi kujitosheleza, kutojitoshela matamania yenu ya kibinafsi, lakini kumtosheleza Mungu tu, bila ya chaguo lenu la kibinafsi. Je, yupo aliye hivi? Kwa hakika, kunayo hoja moja tu ambayo imewekwa mbele ya macho yenu nyinyi wenyewe. Ni kile ambacho kila mmoja wenu anavutiwa nacho, kile ambacho mnachotaka kujua zaidi, na hilo ni suala la matokeo na hatima ya kila mmoja wenu. Huenda msitambue, lakini hili ni jambo ambalo hakuna anayeweza kulikataa. Ninajua kwamba kunao baadhi ya watu ambao, tunapokuja katika ukweli wa matokeo ya binadamu, ahadi ya Mungu kwa ubinadamu, na aina gani ya hatima ambayo Mungu ananua kumleta binadamu katika, tayari wamefanyia uchunguzi neno la Mungu katika masuala haya mara kadhaa. Kisha kunao ambao kila mara wanalitafuta na kulifikiria kwenye akili zao, na bado hawapati matokeo, au pengine wanafikia katika hitimisho fulani isiyoeleweka. Hatimaye bado hawana hakika kuhusu ni aina gani ya matokeo yanayowasubiri. Wanapotekeleza wajibu wao, baadhi ya watu siku zote wanataka kujua majibu dhahiri kwa maswali yafuatayo: Matokeo yangu yatakuwa yapi? Ninaweza kutembelea njia hii hadi mwisho wake? Mwelekeo wa Mungu kwake binadamu ni upi? Baadhi ya watu huwa hata na wasiwasi: Nimefanya baadhi ya mambo siku zilizopita, nimesema baadhi ya mambo, sikumtii Mungu, nimefanya mambo fulani ambayo yamemsaliti Mungu, kulikuwa na masuala fulani ambapo sikumtosheleza Mungu, niliumiza moyo wa Mungu, nilimfanya Mungu kunikasirikia, nilimfanya Mungu kunichukia na kuniona

kwamba ninachukiza, hivyo basi pengine matokeo yangu hayajulikani. Ni haki kusema kwamba watu wengi zaidi wanahisi wasiwasi kuhusu matokeo yao wenyewe. Hakuna anayethubutu kusema: “Nahisi kwa uhakika wa asilimia mia moja kwamba nitaishi Ninao uhakika wa asilimia mia moja kwamba ninaweza kuzitosheleza nia za Mungu; mimi ni mtu anayefuata moyo wa Mungu; mimi ni mtu anayesifiwa na Mungu.” Baadhi ya watu hufikiria ni vigumu hasa kufuata njia ya Mungu, na kwamba kutia ukweli katika matendo ndilo jambo gumu zaidi la kufanya. Kwa hivyo, watu hawa hufikiria hawawezi kusaidika, na hawathubutu kuwa na matumaini ya kuwa na matokeo mazuri. Au pengine wanasadiki kwamba hawawezi kutosheleza nia za Mungu, na kuweza kuishi; na kwa sababu ya haya watasema kwamba hawana matokeo, na hawawezi kufikia hatima nzuri. Licha ya jinsi watu hufikiria, kila mmoja anastaajabu kuhusu matokeo yao mara nyingi. Kuhusu masuala ya siku zao za usoni, kuhusu maswali ya kile watakachopata wakati Mungu atakapomaliza kazi Yake, watu hawa siku zote wanapiga hesabu, siku zote wanapanga. Baadhi ya watu wanalipia bei mara dufu; baadhi ya watu wanaacha familia zao na kazi zao; baadhi wanakata tamaa katika ndoa zao; baadhi yaowanakubali bila kulalamika kujitumia kwa ajili ya Mungu; baadhi ya watu huacha nyumba zao ili kutenda wajibu wao; baadhi ya watu huchagua ugumu, na kuanza kufanya kazi ambazo ni chungu zaidi na zinachosha zaidi; baadhi ya watu huchagua kuutoa utajiri wao, kujitolea kila kitu chao; na bado baadhi ya watu huchagua kufuata ukweli na kufuatilia kumjua Mungu. Haijalishi namna mnavyochagua kutenda, namna mnavyotenda ndiyo muhimu zaidi? (Si muhimu.) Ni vipi tunavyoelezea kwamba si muhimu, basi? Kama namna hiyo si muhimu, basi ni nini muhimu? (Tabia nzuri kwa nje si wakilishi wa kutia ukweli katika matendo.) (Kile ambacho kila mmoja anafikiria si muhimu. Cha msingi hapa ni kama tumeweza kutia ukweli katika matendo, na kama tunampenda Mungu.) (Maangamizi ya wapinga Kristo na viongozi bandia hutusaidia kuelewa kwamba tabia ya nje si jambo muhimu zaidi. Kwa nje wanaonekana kuwa wamejinyima mengi, na wanaonekana kuwa radhi kulipa bei, lakini kwa kuchambua tunaweza kuona kwamba hawana moyo kabisa unaomcha Mungu; kwa mitazamo yote wanampinga Yeye. Siku zote wanasimama pamoja na Shetani katika nyakati za hatari, na kuingilia kazi ya Mungu. Hivyo basi, utiliaji maanani mkuu hapa ni upande gani tutasimama wakati ukiwadia, na mitazamo yetu.) Nyote mnaongea vyema, na yaonekana kwamba tayari mnao msingi wa uelewa wa na kiwango cha kuweza kutia ukweli wenu katika matendo, nia za Mungu, na kile Mungu anahitaji kutoka kwa binadamu. Kwamba mnaweza kuongea hivi ni jambo la kugusa kweli. Ingawa kuna maneno machache yasiyofaa hapa na pale, kauli zenu tayari zinakaribia ufafanuzi unaostahili ukweli Hii inathibitisha kwamba mmeimarisha uelewa wenu halisi wa watu matukio, na vifaa vilivyo karibu nanyi, mazingira yenu yote ambayo Mungu amepanga, na kila kitu mnachoweza kuona. Uelewa huu unakaribia ukweli. Hata ingawa kile mnachosema si pana kabisa, na maneno machache hayafai sana, uelewa wenu tayari unakaribia uhalisi wa ukweli. Kuwasikiliza mkiongea kwa njia hii kunanifanya

Mimi kuhisi vizuri sana.

Imani za Watu Haziwezi Kubadilishwa na Ukweli

Kunao baadhi ya watu wanaoweza kuvumilia ugumu; wanaweza kulipia bei; tabia yao ya nje ni nzuri sana; wanaheshimika sana; na wanatamaniwa na wengine. Mnafikiria nini: Je, tabia kama hii ya nje inaweza kuchukuliwa kama ya kutia ukweli katika matendo? Mnaweza kusema kwamba mtu huyu anatosheleza nia za Mungu? Kwa nini mara kwa mara watu wanamwona mtu wa aina hii na kufikiria kwamba wao wanamtosheleza Mungu, wanafikiria kwamba wanatembelea njia ile ya kutia ukweli katika matendo, kwamba wanatembea katika njia ya Mungu? Kwa nini baadhi ya watu hufikiria kwa njia hii? Upo ufafanuzi mmoja tu kwa haya. Na ufafanuzi huu ni upi? Sababu ni kwamba kwa kiasi kikubwa cha watu, maswali kama kutia ukweli katika matendo ni nini, kutosheleza Mungu ni nini, ni nini kuwa na uhalisia wa ukweli—maswali haya hayako wazi sana. Hivyo basi kunao baadhi ya watu ambao mara nyingi wanadanganywa na wale ambao kwa nje wanaonekana wa kiroho, wanaonekana wa kilodi, wanaonekana kuwa na taswira za ukuu. Kuhusiana na watu hao wanaoweza kuzungumzia barua na falsafa, na ambao hotuba na vitendo vyao vinaonekana kuwa vyenye kustahili uvutiwaji, wale wanaodanganywa nawao hawajawahi kuangalia kiini halisi cha vitendo vyao, kanuni zinazoendesha vitendo vyao, au shabaha zao ni nini. Na hawajawahi kuangalia kama watu hawa wanatii Mungu kwa kweli, na kama wao ni watu wanaomcha Mungu kwa kweli na kujiepusha na uovu au la. Hawajawahi kutambua kile kiini halisi cha ubinadamu cha watu hawa. Badala yake, kutoka kwenye hatua ya kwanza ya kujua na kuzoeana nao, hatua kwa hatua wanaanza kuwapenda watu hawa, kuwatukuza watu hawa, na hatimaye watu hawa wanakuwa sanamu zao. Aidha, katika akili za baadhi ya watu, sanamu hizi wanazoziaibu, wanaosadiki wanaweza kuacha familia na kazi zao, na kulipa ile bei kwa juujuu—sanamu hizi ndizo ambazo kwa kweli zinatosheleza Mungu, ndizo zile zinazoweza kupokea kwa kweli matokeo mazuri na hatima nzuri. Katika akili zao, sanamu hizi ndizo wale watu ambao Mungu husifu. Ni nini husababisha watu kuwa na aina hii ya kusadiki? Ni nini kiini halisi cha suala hili? Ni nini matokeo hali hii inaweza kuleta? Hebu na tuzungumzie kwanza suala la kiini chake halisi.

Masuala haya kuhusiana na mitazamo ya watu, vitendo vya watu, ni kanuni gani ambazo watu wanachagua kutenda, na kile ambacho kwa kawaida kila mtu anatilia mkazo, kimsingi haya yote hayahusu mahitaji ya Mungu kwa mwanadamu hata kidogo. Bila kujali kama watu wanazingatia masuala ya juujuu au yale ya kina, wanazingatia barua na falsafa au uhalisia, watu hawatii yale ambayo wanafaa kutii zaidi, na hawajui kile wanachofaa kujua zaidi. Sababu ya hali hii kuwa hivi ni kwamba watu hawaupendi ukweli kamwe. Hivyo basi, watu hawako radhi kutumia muda na jitihada zao katika kutafuta na kuendeleza kanuni katika neno la Mungu.

Badala yake, wanapendelea kutumia njia za mkato, na kujumlisha kile wanachoelewa, kile wanachojua, kuwa vitendo vizuri na tabia nzuri. Muhtasari huu nao huwa shabaha yao ya binafsi ya kufuata, unakuwa ukweli wa kutendwa. Athari ya moja kwa moja ya haya yote ni kwamba watu wanatumia tabia nzuri ya kibinadamu kama kisawazisho cha kutia ukweli katika matendo yao, hali ambayo inatosheleza pia matamania ya watu ili kupata fadhila na Mungu. Hii inawapa watu mtaji wa kushindania ukweli, ambao pia wao hutumia kutoa sababu na kushindana na Mungu. Wakati uo huo, watu wanamweka Mungu kando kwa njia za ufidhuli, na kuiweka ile sanamu ya mioyo yao katika nafasi ya Mungu. Kunayo sababu moja tu ya chanzo cha haya ambayo huwafanya watu kuwa na vitendo wasivyovijua, mitazamo wasiyovijua, au mitazamo na vitendo vya upande mmoja, na leo Nitawaelezea kuhusu haya. Sababu ni kwamba ingawa watu wengi wanaweza kumfuata Mungu, kumwomba Yeye kila siku, na kusoma neno la Mungu kila siku, hawaelewi kwa hakika nia za Mungu. Hiki ndicho chanzo cha tatizo. Kama mtu huelewa moyo wa Mungu, huelewa kile anachopenda Mungu, kile humchukiza Mungu, kile anachotaka Mungu, kile anachokataa Mungu, ni mtu wa aina gani ambaye Mungu humpenda, ni mtu wa aina gani ambaye Mungu hampendi, ni kiwango kipi ambacho Mungu hutumia katika kutoa mahitaji Yake kwa binadamu, ni mtazamo gani ambao Anauchukua katika kumfanya binadamu kuwa mtimilifu, je, mtu huyu anaweza bado kuwa na mawazo yake ya kibinafsi? Wanaweza tu kuenda na kumwabudu mtu mwingine? Mtu wa kawaida anaweza kuwa sanamu yao? Kama mtu anaelewa nia za Mungu, mtazamo wake ni wenye kirazini zaidi kuliko hapo. Hawatamwabudu kama Mungu kiongozi aliyepotoka kiholela, wala hawataweza, huku wakitembea njia ya kutia ukweli katika matendo, kusadiki kwamba kutii kiholela katika sheria au kanuni chache rahisi ni sawa na kutia ukweli katika matendo.

Kunayo Maoni Mengi Yanayohusu Kiwango Ambacho Mungu Hutumia Kuasisi Matokeo ya Binadamu

Hebu na turudi katika mada hii na tuendeleo kuzungumzia suala la matokeo.

Kwa sababu kila mmoja anajali matokeo yake, je, mnajua namna ambavyo Mungu huamua matokeo hayo? Na ni kwa njia gani ambayo Mungu huanzisha matokeo ya mtu? Na ni kiwango gani ambacho Mungu hutumia kuasisi matokeo ya mtu? Na wakati ambapo matokeo ya mtu yangali bado hayajaasisiwa, ni nini anachofanya Mungu ili kufichua matokeo haya? Je, yupo anayejua haya? Kama Nilivyosema tu, kuna baadhi ambao tayari wamefanyia uchunguzi neno la Mungu kitambo sana. Watu hao wanatafuta dalili fulani kuhusu matokeo ya mwanadamu, kuhusu kategoria ambazo matokeo haya yamegawanywa, na kuhusu matokeo tofauti yanayosubiria aina tofauti ya watu. Wanataka pia kujua namna neno la Mungu linavyoanzisha matokeo ya binadamu, aina za kiwango ambacho Mungu hutumia, na njia ambayo Yeye huasisi

matokeo ya binadamu. Ilhali mwishowe watu hawa hawafanikiwi kupata chochote. Kwa hakika, yapo mambo machache yenye thamani yanayozungumzwa kuhusu suala hili miongoni mwa neno la Mungu. Kwa nini hali iko hivi? Ili mradi matokeo ya binadamu yangali hayajafichuliwa, Mungu hataki kumwambia yeyote kuhusu kile kitakachofanyika mwishowe, wala Hataki kumfahamisha yeyote kuhusu hatima yao kabla ya wakati kufika. Sababu ya kufanya hivi ni kwamba Mungu kufanya hivyo hakutaleta manufaa yoyote kwa binadamu. Sasa hivi, Nataka kuwaambia tu kuhusu namna Mungu huasisi matokeo ya binadamu, kuhusu kanuni Anazotumia katika kazi Yake ili kuyaasisi matokeo ya binadamu, na kuonyesha matokeo haya, pamoja na kiwango Anachotumia ili kuanzisha kama mtu ataweza kuishi au la. Hiki sicho kile ambacho mnajali zaidi kuhusu? Hivyo basi, ni vipi ambavyo watu hufahamu njia ambayo Mungu anaanzisha matokeo ya binadamu? Mlizungumzia kidogo kuhusu suala hili muda mfupi uliopita. Baadhi yenu mlisema kwamba ni swali la kutenda wajibu wao kwa uaminifu, kugharamika kwa ajili ya Mungu; baadhi ya watu walisema kumtii Mungu na kutosheleza Mungu; baadhi ya watu walisema kudhibitiwa na Mungu; na baadhi ya watu walisema kuishi maisha ya hadhi ya chini.... Wakati mnapotia ukweli huu katika matendo, wakati mnapotenda kanuni za kufikiria kwenu, je mnajua kile Mungu anachofikiria? Mmewahi kufikiria kama kuendelea hivi ni kutosheleza nia za Mungu au la? Kama kunatilia maanani kiwango cha Mungu? Kama kunatilia maanani mahitaji ya Mungu? Ninasadiki kwamba watu wengi zaidi hawalifikirii suala hili kwa undani. Wanatumia tu bila kutilia maanani sehemu ya neno la Mungu, au sehemu ya mahubiri, au viwango vya watu fulani wa kiroho ambao wanawaabudu, na kujilazimisha kufanya hivi na vile. Wanasadiki kwamba hii ndiyo njia sahihi, na hivyo basi wanaendelea kuitii, kuifanya, liwalo liwe hatimaye. Baadhi ya watu hufikiria: “Nimesadiki kwa miaka mingi siku zote nimetenda mambo kwa njia hii; nahisi kuwa nimemtoshesheleza kabisa Mungu; ninahisi pia kuwa nimejifunza mengi kutoka kwa haya. Kwani nimekwishaelewa ukweli mwingi katika kipindi hiki, na nimeelewa mambo mengi ambayo sikuyaelewa awali—hasa, wingi wa fikira na mitazamo yangu imebadilika, maadili ya maisha yangu yamebadilika sana, na ninao uelewa mzuri sana wa ulimwengu huu.” Watu kama hao wanasadiki kwamba haya ni mavuno, na ndiyo matokeo ya mwisho ya kazi ya Mungu kwa binadamu. Kwa maoni yenu, kwa viwango hivi na vitendo vyenu nyote vimewekwa pamoja—je, mnatosheleza nia za Mungu? Baadhi ya watu watasema kwa uhakika wote: “Bila shaka! Tunatenda kulingana na neno la Mungu; tunatenda kulingana na kile ambacho yule aliye juu alihubiri na kushiriki nasi; siku zote tunafanya wajibu wetu, siku zote tunamfuata Mungu, hatujawahi kumwacha Mungu. Hivyo basi tunaweza kusema kwa imani kamili kwamba tunamtoshesheleza Mungu. Haijalishi ni kiasi kipi tunachoelewa kuhusu nia za Mungu, haijalishi ni vipi tunavyoelewa neno la Mungu, siku zote tumekuwa kwa njia ya kutafuta kuweza kutangamana na Mungu. Kama tutachukua hatua kwa usahihi, na kutenda kwa usahihi, basi matokeo yatakuwa sahihi.” Je, mnafikiria nini kuhusu mtazamo huu? Je, ni kweli?

Pengine wapo wale wanaosema: “Sijawahi kufikiria kuhusu mambo haya awali. Mimi nafikiria tu kwamba nikiendelea kutimiza wajibu wangu na kuendelea kutenda kulingana na mahitaji ya neno la Mungu, basi nitasalia. Sijawahi kufikiria swali la kama ninaweza kutosheleza moyo wa Mungu, na sijawahi kufikiria kama ninatimiza kiwango kinachohitajika na Yeye. Kwa sababu Mungu hajawahi kuniambia, wala kunipatia maagizo yoyote kwa uwazi, ninasadiki kwamba mradi tu niendeleo kupiga hatua mbele, Mungu atatosheka na Yeye hafai kuwa na mahitaji yoyote ya ziada kwangu mimi.” Je, kusadiki huku ni sahihi? Kulingana na Ninavyojua, njia hii ya kutenda, njia hii ya kufikiria, na mitazamo hii—yote yanakuja na madoido fulani na kiasi kidogo cha upofu. Ninaposema hivi, pengine wapo baadhi yenu mnaohisi kuvunjika moyo: “Yaani upofu? Kama ni ‘upofu,’ basi tumaini letu la wokovu, tumaini letu la kuishini dogo mno, na halina uhakika, hapo ni kweli? Je, wewe kulitamka hivyo lilivyo si sawa na kutumwagilia maji baridi?” Hajjalishi kile mnachosadiki, mambo Ninayoyasema na kufanya hayanuii kukufanya ninyi kuhisi kama mnamwagiliwa maji baridi. Badala yake, yananua kuboresha uelewa wenu wa nia za Mungu, na kuboresha ung’amuzi wenu kuhusu kile ambacho Mungu anafikiria, kile ambacho Mungu anataka kukamilisha ni mtu wa aina gani ambaye Mungu anapenda, nini kinachukiza Mungu, nini Mungu anadharau, ni mtu wa aina gani ambaye Mungu anataka kumpata, na ni mtu wa aina gani ambaye Mungu anatupilia mbali. Yananua kupatia akili zenu uwazi, kuwasaidia kujua wazi ni kiwango kipi vitendo na fikira za kila mmoja wenu yamepotea kutoka kwa kiwango kinachohitajika na Mungu. Je, inahitajika kuzungumzia mada hii? Kwa sababu Ninajua mmesadiki kwa muda mrefu, na mmesikiliza mahubiri mengi, lakini kwa hakika haya ndiyo mambo yanayokosekana zaidi. Mmerekodi kila ukweli katika daftari zenu, mmerekodi pia kile ambacho nyie wenyewe mnasadiki kibinafsi kuwa muhimu katika akili zenu na ingawa mnapanga kutumia haya kumridhisha Mungu wakati wa kutenda kwenu, kuyatumia mnajipata mkihitaji msaada, kuyatumia kupitia nyakati ngumu zilizo mbele yenu, au mnaacha ukweli huu uandamane na ninyi mnapoishi maisha yenu tu. Lakini kulingana na Ninavyojua, iwapo mnatenda tu, namna mnavyotenda hasa si muhimu. Nini, basi, ndicho kitu cha muhimu sana? Ni kwamba wakati unatenda, moyo wako hujua kwa uhakika wote kama kila kitu unachofanya, kila kitendo, ndicho kile anachotaka Mungu au la; kama kila kitu unachofanya ni sahihi au la, kila kitu unachofikiria ni sahihi au la, na matokeo na shabaha katika moyo wako yanatosheleza nia za Mungu au la, kama yanatilia maanani mahitaji ya Mungu au la, na kama Mungu anayaidhinisha au la. Haya ni mambo muhimu.

Tembea katika Njia ya Mungu: Mche Mungu na Kuepuka Maovu

Kunao msembo ambao mnafaa kutilia maanani. Ninasadiki msembo huu ni muhimu sana, kwa sababu kwangu Mimi unakuja akilini mara nyingi kila siku. Kwa nini hivyo? Kwa sababu kila wakati Ninapokumbana na mtu, kila wakati Ninaposikia hadithi ya mtu, kila wakati Ninaposikia

kile alichopitia mtu au ushuhuda wake wa kusadiki Mungu, siku zote Ninatumia msemu huu kuweza kupima kama mtu huyu binafsi ni mtu wa aina ambayo Mungu anataka au la, mtu wa aina ambayo Mungu anapenda. Hivyo msemu huu ni upi, basi? Sasa nyinyi nyote mnasubiri kwa hamu. Nitakapoufichua msemu huu, pengine mtakasirika kwa sababu wapo baadhi yenu ambao mmekuwa mkijifanya kuwa mnakubaliana nao kwa miaka mingi. Lakini Kwangu Mimi, Sijawahi kujifanya kuwa nakubaliana nao. Msemu huu umo moyoni Mwangu. Hivyo basi msemu huu ni upi? Msemu ni “tembea katika njia ya Mungu: mche Mungu na kuepuka maovu.” Je, huoni kwamba kauli hii ni rahisi kupindukia? Ilhali ingawa msemu huu unaweza kuwa rahisi, mtu ambaye anao uelewa wa ndani na wa kweli wa msemu huu atahisi kwamba ni wenye uzito mkubwa; kwamba unao thamani nyingi ya kutenda; kwamba ni lugha ya uzima iliyo na uhalisia wa ukweli; ambayo ni lengo la maishani katika kulenga wale wanaotafuta kutosheleza Mungu; na hiyo ni njia ya maisha marefu itakayofuatwa na mtu yeyote anayejali nia za Mungu. Hivyo basi mnafikiria nini: Je, msemu huu sio ukweli? Je, unao umuhimu kama huo au la? Pia, pengine baadhi yenu mnafikiria kuhusu msemu huu, wakijaribu kuuelewa, na wapo baadhi ambao bado wanautilia shaka. Je, msemu huu ni muhimu sana? Je, ni muhimu sana? Unahitajika sana na unastahili kutiliwa mkazo? Pengine wapo baadhi ya watu ambao hawapendi sana msemu huu kwa sababu wanafikiria kwamba kuchukua njia ya Mungu na kuitiririsha ndani ya msemu huu mmoja ni urahisishaji wa kupindukia. Kuyachukua yale yote ambayo Mungu alisema na kuyafanya yawe msemu mmoja—je, hivi si kumfanya Mungu kuwa yule asiyekuwa na umuhimu sana? Hivi ndivyo ilivyo? Inaweza kuwa kwamba wengi wenu nyinyi hamwelewi kabisa maana kuu ya maneno haya. Ingawa mmeyanakili na kuyatilia maanani, hamnuii kuuweka msemu huu katika mioyo yenu; mnaunakili tu katika vitabu vyenu, na kuudurusu tu, na kuufikiri katika muda wenu wa ziada. Wapo baadhi ya watu ambao hata hawatashughulika kuutia kwenye kumbukumbu msemu huu, sikuambii hata kujaribu kuutumia vizuri. Lakini kwa nini Nikauzungumzia msemu huu? Licha ya mtazamo wenu, au kile mtakachofikiria, lazima Nizungumzie msemu huu kwa sababu unafaa ajabu namna ambavyo Mungu huasisi matokeo ya binadamu. Bila kujali kama uelewa wenu wa sasa wa msemu huu upo, namna mnavyouchukulia, bado Nitawaeleza: kama watu wanaweza kuyaweka maneno ya msemu huu katika vitendo na kuyapitia, na kutimiza kiwango cha kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, basi atahakikishiwa kuishi kisha atahakikishiwa kuwa mtu mwenye matokeo mazuri. Kama huwezi kutimiza kiwango kilichowekwa wazi katika msemu huu, basi inaweza kusemekana kwamba matokeo yako hayajulikani. Hivyo basi Ninaongea kwenu kuhusu msemu huu kwa matayarisho yenu ya kiakili, na ili mjue ni kiwango aina gani ambacho Mungu anatumia kuwapima. Kama Nilivyozungumza tu muda mfupi uliopita, msemu huu unafaa pakubwa kwa wokovu wa Mungu kwa binadamu na namna ambavyo Aliyaasisi matokeo ya binadamu. Uhusiano huu unapatikana wapi? Mngependa kwa kweli kujua, hivyo basi tutauzungumzia leo.

Mungu Hutumia Majaribio Tofauti ili Kupima Kama Watu Humcha Mungu na Kujiepusha na Maovu

Katika kila enzi, Mungu huwapa binadamu baadhi ya maneno Anapofanya kazi ulimwenguni, huku akimwambia mwanadamu kuhusu baadhi ya ukweli. Ukweli huu unahudumu kama njia ambayo binadamu anafaa kuitii, njia ya kutembelewa na binadamu, njia ambayo humwezesha binadamu kumcha Mungu na kujiepusha na uovu, na njia ambayo watu wanafaa kuweka katika vitendo na kuitii katika maisha yao na kwenye mkondo wa safari zao za maisha. Ni kwa sababu hizi ambapo Mungu anampa binadamu maneno haya. Binadamu anafaa kuyatii maneno haya yanayotoka kwa Mungu, na kuyatii ni kupokea uzima. Kama mtu hataweza kuyatii, na hayatii kwenye matendo, na haishi kwa kudhihirisha maneno ya Mungu katika maisha yake, basi mtu huyo hautilii ukweli katika matendo. Na kama hawatilii ukweli katika matendo, basi hawamchi Mungu na hawaepuki uovu, wala hawawezi kumtosheleza Mungu. Kama mtu hawezi kumtosheleza Mungu, basi hawezi kupokea sifa ya Mungu; mtu wa aina hii hana matokeo. Hivyo basi ni vipi katika mkondo wa kazi ya Mungu ndipo Anapoasisi matokeo ya mtu? Ni mbinu gani anayoitumia Mungu kuasisi matokeo ya binadamu? Pengine nyinyi hamlielewi suala hili sasa hivi, lakini Nitakapowaambia mchakato jambo hili litakuwa wazi kabisa. Hii ni kwa sababu watu wengi tayari wamelipitia suala hili wenyewe.

Katika mkondo wa kazi ya Mungu, kuanzia mwanzo hadi sasa, Mungu Amapanga majaribio kwa kila mtu—au mnaweza kusema, kila mtu anayemfuata Yeye—na majaribio haya yanakuja kwa ukubwa tofauti. Wapo wale ambao wamepitia jaribio la kukataliwa na familia zao; wapo wale ambao wamepitia jaribio la mazingira mabovu; wapo wale ambao wamepitia majaribio ya kukamatwa na kuteswa; wapo wale ambao wamepitia majaribio ya kukumbwa na chaguo; na wapo wale ambao wamekumbwa na majaribio ya pesa na hadhi. Nikizungumza kwa ujumla, kila moja wenu amekabiliwa na aina zote za majaribio. Kwa nini Mungu anafanya kazi hivyo? Kwa nini Mungu Anamtenda hivi kila mtu? Ni matokeo aina gani Anayotaka kuyaona? Hii ndiyo hoja muhimu kuhusu kile Ninachotaka kuwaambia: Mungu anataka kuona kama mtu huyu ni yule anayemcha Mungu na kujiepusha na uovu. Maana ya haya ni kwamba wakati Mungu anakupa jaribio, na kukufanya kukabiliwa na baadhi ya hali, Anataka kukupima na kujua kama wewe ndiye yule mtu anayemcha Mungu, mtu huyo anayejeiepusha na uovu au la. Kama mtu amekumbwa na wajibu wa kutunza sadaka, na anakutana na sadaka ya Mungu, basi unadhani kwamba hiki ni kitu ambacho Mungu amepanga? Bila shaka! Kila kitu unachokumbana nacho ni kitu ambacho Mungu amepanga. Unapokumbwa na suala hili, Mungu atakuangalia kwa siri, namna ulivyochagua, namna unavyotenda, na kile unachofikiria. Matokeo yake ya mwisho ndiyo ambayo Mungu anayajali zaidi, sababu ni matokeo ambayo yatamruhusu Yeye kupima kama umetimiza kiwango cha Mungu katika jaribio hilo au la. Hata hivyo, wakati

watu wanapokumbwa na baadhi ya masuala haya, mara nyingi hawafikirii kuhusu ni kwa nini wanakumbwa na mambo hayo, au kile kiwango ambacho kinahitajika na Mungu. Hawafikirii kuhusu kile Mungu anachotaka kutoka kwao, kile Anachotaka kupata kutoka kwao. Wakati wanapokumbwa na suala hili, mtu wa aina hii anafikiria tu: “Hili ni jambo ambalo nimekumbwa nalo; lazima niwe makinifu, wala si mzembe! Haijalishi ni nini, hii ni sadaka ya Mungu na siwezi kuigusa.” Mtu huyo anasadiki kwamba anaweza kutimiza jukumu lake kupitia kufikiria huko sahili. Je, Mungu ataweza kutosheka na matokeo ya jaribio hili? Au Hatatosheka? Mnaweza kuzungumzia suala hili. (Kama mtu anamcha Mungu katika moyo wake, kisha anapokumbwa na wajibu unaomruhusu kukutana na sadaka ya Mungu, anaweza kufikiria namna ilivyo rahisi kukosea tabia ya Mungu, ili wawe na hakika ya kuendelea kwa tahadhari.) Mwitikio wako u katika njia sahihi, lakini bado haujafika. Kutembea katika njia ya Mungu hakuhusu kuangalia sheria juujuu. Badala yake, kunamaanisha kwamba unapokabiliwa na suala, kwanza kabisa, unaliangalia kama ni hali ambayo imepangwa na Mungu, wajibu uliopewa wewe na Yeye, au kitu ambacho Amekuaminia wewe, na kwamba unapokabiliana na suala hili, unapaswa kuliona kama jaribio kutoka kwa Mungu. Wakati unapokabiliwa na suala hili, lazima uwe na kiwango, lazima ufikirie kwamba suala hilo limetoka kwa Mungu. Lazima ufikirie ni vipi ambavyo utashughulikia suala hili kiasi cha kwamba unaweza kutimiza wajibu wako, na kuwa mwaminifu kwa Mungu; namna ya kulifanya bila ya kumghadhabisha Mungu; au kukosea tabia Yake. Tumetoka tu kuzungumzia kutunza sadaka. Swala hili linahusu sadaka, na linahusisha pia wajibu wako, jukumu lako. Unahitajika kuwajibikia jukumu hili. Ilhali unapokabiliwa na suala hili, kunalo jaribio lolote? Lipo! Jaribio hilo linatoka wapi? Jaribio hilo linatoka kwa Shetani, na linatoka pia kwa tabia potovu na ya uovu ya binadamu. Kwa sababu kunalo jaribio, hili linahusisha kuwa shahidi; kuwa shahidi ni jukumu na wajibu wako pia. Baadhi ya watu husema: “Hili ni suala dogo; kwa kweli linahitajika kulifanya suala hili dogo kuwa kubwa hivyo?” Ndiyo pana haja! Kwa sababu ili kutembea katika njia ya Mungu, hatuwezi kuwachilia chochote kinachotuhusu sisi wenyewe, au kinachofanyika karibu nasi, hata yale mambo madogo madogo. Haijalishi kama tunafikiria tunafaa kumakinika au la, mradi tu suala lolote linatukabili hatufai kuliacha. Lote linafaa kuonekana kama jaribio la Mungu kwetu. Mwelekeo aina hii uko vipi? Kama unao mwelekeo aina hii, basi unathibitisha hoja moja: Moyo wako unamcha Mungu, na moyo wako uko radhi kujiepusha na maovu. Kama unalo tamanio hili la kumtosheleza Mungu, basi kile unachotia katika matendo hakiko mbali na kiwango cha kumcha Mungu na kujiepusha na maovu.

Kunao mara nyingi wale wanaosadiki kwamba masuala ambayo hayatiliwi maanani na watu, masuala ambayo kwa kawaida hayatajwi—haya ni mambo madogo tu, na hayana chochote kuhusiana na kutia ukweli katika matendo. Wakati watu hawa wanakabiliwa na suala kama hilo,

hawalifikirii sana na wanaliachilia tu. Lakini ukweli wa mambo ni kwamba, suala hili ni funzo ambalo unafaa kulidadisi, funzo kuhusu namna ya kumcha Mungu, namna ya kujiepusha na maovu. Zaidi, kile unachofaa kujali hata zaidi ni kujua kile Mungu anachofanya wakati suala hili linapoibuka kukabiliana na wewe. Mungu yuko kando yako, anaangalia kila mojawapo ya maneno na vitendo vyako, anaangalia hatua zako, mabadiliko ya akili zako—hii ni kazi ya Mungu. Baadhi ya watu husema: “Basi kwa nini siihisi?” Huihisi kwa sababu namna ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu haijawa ndiyo njia muhimu zaidi kwako kushughulikiwa. Hivyo basi, huwezi kuhisi kazi ngumu ya Mungu katika binadamu, inayojionyesha kulingana na fikira tofauti na vitendo tofauti vya watu. Wewe u makini! Suala kubwa ni lipi? Swala dogo ni lipi? Masuala yote yanayohusu kutembea katika njia ya Mungu hayagawanywi kwa masuala makubwa au madogo. Mnaweza kulikubali hilo? (Tunaweza kulikubali.) Kuhusiana na masuala ya kila siku, kunayo yale ambayo watu wanayaona kuwa makubwa sana na muhimu, na mengine yanaonekana kuwa mambo madogo madogo tu. Mara nyingi watu huyaona masuala haya makubwa kuwa ndiyo muhimu zaidi, na wanayachukulia kwamba yametumwa na Mungu. Hata hivyo, kwenye mkondo wa masuala haya makubwa kujitokeza, kutokana na kimo finyu cha binadamu, na kutokana na kiwango cha binadamu kisichotosha, mara nyingi binadamu haendani sawa na nia za Mungu, hawezi kupata ufunuo wowote, na hawezi kufaidi maarifa yoyote halisi yenye thamani. Kuhusu masuala madogo, haya yanapuuzwa tu na binadamu, kuachwa kuponyoka kidogokidogo. Hivyo basi, wamepoteza fursa nyingi sana za kuchunguzwa mbele ya Mungu, kujaribiwa na Yeye. Je unafaa kuwapuuza watu, masuala na hali hizi siku zote ambazo Mungu anakupangilia wewe, hii itamaanisha nini? Inamaanisha kwamba kila siku, hata kila wakati, siku zote unakana ukamilifu wa Mungu kwako, na uongozi wa Mungu. Kila Mungu anapopanga hali hizi kwako wewe, Yeye anakuangalia kwa siri, Anauangalia moyo wako, Anaziangalia fikira na hali zako, Anaangalia namna unavyofikiria wewe, Anaangalia namna unavyochukua hatua. Kama wewe ni mtu asiyejali—mtu ambaye hajawahi kujali kuhusu njia ya Mungu, neno la Mungu, au ukweli—basi hutajali, hutatilia maanani kile ambacho Mungu anataka kukamilisha, na yale ambayo Mungu anakuhitaji wewe kufanya wakati Anapopanga hali hizi kwako wewe. Hutajua pia namna ambavyo masuala haya ya kila siku yanavyohusiana na ukweli au nia za Mungu. Baada ya kukabiliana na hali nyingi kama hizi na majaribio mengi kama haya, huku naye Mungu haoni mafanikio yoyote kutokana na wewe, ataweza kuendelea vipi? Baada ya kukabiliwa na majaribio mara kwa mara, humkuzi Mungu katika moyo wako, na hushughulikii zile hali ambazo Mungu anakupangia wewe kama zilivyo—kama majaribio ya Mungu au mitihani ya Mungu. Badala yake unakataa fursa ambazo Mungu amekupa wewe moja baada ya nyingine, na unaziacha kutokomea mara kwa mara. Je huu si kutotii kwa kiwango cha juu na binadamu? (Naam, ni kutotii.) Je, Mungu atahuzunika kwa sababu ya haya? (Naam Atahuzunika.) Mungu hatahuzunika! Mkinisikia Nikiongea hivi mnashtuka kwa mara nyingine

tena. Kwani umesahau, ilisemekana hapo awali kwamba Mungu huhuzunika siku zote? Mungu hatahuzunika? Ni lini basi Mungu atahuzunika? Usijali, Mungu hatahuzunika na hali hii. Basi mwelekeo wa Mungu kwa aina hii ya tabia iliyoelezwa kwa muhtasari hapo juu ni upi? Wakati watu wanapokataa majaribio, mitihani, ambayo Mungu anawapa, wakati wanapoikwepa, kuna mwelekeo mmoja tu ambao Mungu anao kwa watu kama hawa. Mwelekeo huu ni upi? Mungu husukumia mbali aina hii ya watu kutoka kina cha moyo Wake. Kunazo safu mbili za maana ya kauli “sukumia mbali”. Ninawezaje kuzielezea? Ndani kabisa ya moyo, kauli hii inao mkazo wa kuchukiza, wa chuki. Na je, safu ya pili ya maana? Sasa hiyo ndiyo sehemu inayoashiria kukata tamaa dhidi ya kitu. Nyote mnajua “kukata tamaa” kunamaanisha nini, ni kweli? Kwa ufupi, kusukumia mbali kunamaanisha uamuzi na mwelekeo wa mwisho wa Mungu kwa watu wanaokuwa na mwenendo huu. Ni chuki ya kupindukia dhidi yao, maudhi, na hivyo basi uamuzi wa kuwaacha. Huu ndio uamuzi wa mwisho wa Mungu kwa mtu ambaye hajawahi kutembea katika njia ya Mungu, ambaye hajawahi kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Je, nyote mnaweza kuona sasa umuhimu wa msembo huu Niliouzungumzia?

Sasa mnaelewa mbinu ambayo Mungu hutumia kuasisi matokeo kwa binadamu? (Kupanga hali tofauti kila siku.) Kupangilia hali tofauti—hivi ndivyo watu wanavyoweza kuhisi na kugusa. Basi nia ya Mungu kwa haya yote ni nini? Nia ni kwamba Mungu anataka kumpa kila mmoja wetu majaribio katika njia tofauti, katika nyakati tofauti, na katika sehemu tofauti. Ni dhana zipi za binadamu zinazopimwa katika jaribio? Haijalishi kama wewe ni mtu wa aina ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu katika kila suala unalokabiliwa nalo, unalosikia kuhusu, unaloliona, na unalolipitia wewe binafsi au la. Kila mmoja atakabiliwa na aina ya jaribio, kwa sababu Mungu ni mwenye haki kwa watu wote. Baadhi ya watu husema: “Nimesadiki Mungu kwa miaka mingi; inakuaje kwamba sijawahi kabiliwa na jaribio?” Unahisi hujakabiliwa na jaribio kwa sababu kila wakati Mungu amepanga hali kwako wewe, hujazichukulia hali hizo kwa umakinifu, na hujataka kutembea kwa njia ya Mungu. Hivyo basi huna kamwe hisia zozote za majaribio ya Mungu. Baadhi ya watu husema: “Nimekabiliwa na majaribio machache, lakini sijui njia bora ya kufanya mazoezi. Hata ingawa nilitenda, bado sijajua kama nilisimama imara wakati huo wa majaribio.” Watu walio na aina hii ya hali bila shaka hawamo katika kundi la walio wachache. Hivyo basi ni nini kiwango ambacho Mungu hupimia watu? Ni vile tu Nilivyosema muda mfupi uliopita: Kila kitu unachofanya, kila kitu unachofikiria, na kila kitu unachoelezea—ni kumcha Mungu na kujiepusha na uovu? Hivi ndivyo inavyobainika kama wewe ni mtu unayemcha Mungu na kujiepusha na maovu au la. Hii ni dhana rahisi? Ni rahisi mno kusema, lakini ni rahisi pia kutia katika matendo? (Si rahisi mno.) Kwa nini si rahisi mno? (Kwa sababu watu hawamjui Mungu, hawajui namna ambavyo Mungu humfanya binadamu kuwa mtimilifu, na hivyo basi wanapokabiliwa na masuala hawajui namna ya kutafuta ukweli ili

kutatua tatizo lao; watu lazima wapitie majaribio mbalimbali, usafishaji, kuadibu, na hukumu kabla ya kuwa na uhalisia wa kumcha Mungu.) Mnasema hivyo, lakini kulingana na vile mnavyojua, kumcha Mungu na kujiepusha na maovu kunaonekana rahisi kufanywa kwa sasa. Kwa nini Nasema hivi? Kwa sababu mmesikiliza ibada nyingi, na umepokea kiwango kingi cha kunyunyiziwa kwa uhalisia wa ukweli. Hii imewaruhusu kuelewa namna ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu kwa mujibu wa nadharia na kufikiria. Kuhusiana na matendo yenu ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, haya yote yamekuwa yenye manufaa na kuwafanya kuhisi kwamba kitu kama hicho kinaweza kutimizika. Basi ni kwa nini katika uhalisia wa mambo watu hawajawahi kukitimiza? Hii ni kwa sababu kiini halisi cha asili ya binadamu hakimchi Mungu na kinapenda maovu. Hiyo ndiyo sababu halisi.

Kutomcha Mungu na Kutojiepusha na Maovu ni Kumpinga Mungu

Hebu tuanze kuangazia ni wapi ambapo msemu huu “kumcha Mungu na kujiepusha na maovu” ulitokea. (Kitabu cha Ayubu.) Sasa kwa vile mmetaja Ayubu, hebu tumzungumzie. Katika nyakati za Ayubu, Mungu alikuwa akishughulikia kushinda na wokovu wa binadamu? Alikuwa hafanyi hivyo, kweli? Na kuhusiana na Ayubu, ni maarifa kiwango gani alikuwa nayo kumhusu Mungu wakati huo? (Si maarifa mengi.) Na maarifa hayo ya Mungu yanalingana vipi na maarifa mliyo nayo sasa? Inakuwaje kwamba hamthubutu kujibu hili? Maarifa ya Ayubu yalikuwa mengi zaidi au machache kuliko maarifa mliyo nayo sasa? (Machache.) Hili ni swali rahisi sana kujibu. Machache! Hapo nina hakika! Sasa hivi mnaangaliana uso kwa uso na Mungu, uso kwa macho na neno la Mungu. Maarifa yenu ya Mungu ni mengi zaidi kuliko yale ya Ayubu. Kwa nini Naleta suala hili? Kwa nini Ninaongea hivi? Ningependa kuwaelezea hoja moja, lakini kabla Sijafanya hivyo, Ningependa kuwauliza swali: Ayubu alijua machache sana kumhusu Mungu, ilhali angeweza kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Hivyo basi kwa nini watu siku hizi wanashindwa kufanya hivyo? (Upotoshaji mkubwa.) Upotoshaji mkubwa—hicho ndicho kiini cha swali, lakini Sitawahi kulitazama hivyo. Mara nyingi mnachukua falsafa na barua ambazo mnazungumzia mara kwa mara, kama vile “upotoshaji mkuu,” “kuasi dhidi ya Mungu,” “kutotii Mungu,” “kutotii,” “kutopenda ukweli,” na mnatumia vidahizo kama hivi kuelezea kiini halisi cha kila swali. Hii ni njia isiyofaa ya kufanya mazoezi. Kutumia jibu moja kuelezea maswali yaliyo na asili tofauti mara moja huibua shaka ya kuukufuru ukweli na Mungu. Sipendi kusikia aina hii ya jibu. Hebu fikiria! Hakuna yeyote kati yenu amefikiria kuhusu suala hili, lakini kila siku Mimi Ninaliona, na kila siku Mimi Ninalihisi. Hivyo basi, mnafanya, na Mimi Ninatazama. Wakati mnapolifanya, hamwezi kuhisi kiini halisi cha suala hili. Lakini wakati Ninapoliona, Ninaweza kuona kiini halisi chake, na Ninaweza kuhisi kiini chake halisi vilevile. Hivyo basi kiini hiki ni nini basi? Kwa nini watu siku hizi hawamchi Mungu na hawaambai maovu? Majibu yenu yako mbali na kuweza kueleza kiini halisi cha swali hili, na

haziwezi kutatua kiini halisi cha swali hili. Hiyo ni kwa sababu kunacho chanzo hapa ambacho nyinyi hamna habari kukihusu. Chanzo hiki ni kipi? Ninajua mnataka kusikia kukihusu, hivyo basi Nitawaambia kuhusu chanzo cha swali hili.

Hapo mwanzo kabisa wa kazi ya Mungu, Alichukulia vipi binadamu? Mungu alimwoko binadamu; Alimchukulia binadamu kama mmoja wa familia Yake, kama mlengwa wa kazi Yake, kama kile ambacho Alitaka kukishinda, kuokoa, na kile ambacho Alitaka kufanya kuwa kitimilifu. Huu ndio uliokuwa mwelekeo wa Mungu kwa binadamu mwanzoni mwa kazi Yake. Lakini mwelekeo wa binadamu kwa Mungu wakati huo ulikuwa upi? Mungu alikuwa haeleweki kwa binadamu na binadamu alimchukulia Mungu kuwa mgeni. Inaweza kusemwa kwamba mtazamo wao kwa Mungu haukuleta matokeo sahihi, na kwamba hawakuelewa wazi jinsi wanastahili kumshughulikia Mungu. Hivyo basi Alimshughulikia alivyopenda yeye, na akafanya kile alichopenda yeye. Je, binadamu alikuwa na mtazamo kuhusu Mungu? Hapo mwanzoni, binadamu hakuwa na mtazamo wowote kuhusu Mungu. Mtazamo wa binadamu kama ulivyojulikana, ulikuwa tu baadhi ya dhana na fikira kumhusu Mungu. Kile ambacho kiliingiliana na dhana za watu kilikubalika; kile ambacho hakikuingiliana kiliitikiwa juujuu, lakini katika mioyo yao watu waligongana pakubwa nacho na wakakipinga. Huu ndio uliokuwa uhusiano wa binadamu na Mungu hapo mwanzoni: Mungu alimwona binadamu kama mwanachama wa familia, ilhali binadamu alimchukulia Mungu kama mgeni. Lakini baada ya kipindi cha kazi ya Mungu, binadamu alielewa hatimaye kile ambacho Mungu alikuwa akijaribu kutimiza. Watu hatimaye walijua kwamba Mungu ndiye aliyekuwa Mungu wa kweli, na hatimaye wakajua kile ambacho binadamu angpokea kutoka kwa Mungu. Binadamu alimchukulia Mungu wakati huu kuwa nini? Binadamu alichukulia Mungu kuwa tegemeo kuu, akitumai kupokea neema, kupokea baraka, kupokea ahadi. Naye Mungu alimchukulia binadamu wakati huu kuwa nini? Mungu alimchukulia binadamu kuwa mlengwa wa ushindi Wake. Mungu alitaka kuyatumia maneno ili kumhukumu binadamu, kumjaribu binadamu, kumpa majaribio binadamu. Lakini kwa wanadamu wakati huu hasa, Mungu alikuwa kifaa ambacho angetumia kutimiza shabaha zake binafsi. Watu waliona kwamba ukweli uliotolewa na Mungu ungeweza kushinda na kuwaokoa, na kwamba walikuwa na fursa ya kupokea vitu walivyotaka kutoka kwa Mungu, hatima ambayo walikuwa wakitaka. Kwa sababu ya haya, chembechembe ya uaminifu kajitunga katika mioyo yao, na walikuwa radhi kumfuata Mungu huyu. Muda ukapita na watu wakawa na maarifa fulani ya juujuu na ya kifalsafa kuhusu Mungu. Inaweza kusemekana kwamba walikuwa wameanza “kuzoeana” zaidi na zaidi na Mungu. Neno likitamkwa na Mungu, mahubiri Yake, ukweli Aliokuwa ameutoa awali, na kazi Yake—watu walikuwa “wamezoea” zaidi na zaidi. Hivyo basi, watu walidhanja kimakosa kwamba Mungu hakuwa tena mgeni, na kwamba tayari walikuwa wakitembea njia ya uwiano na Mungu. Tangu hapo mpaka sasa, watu

wamesikiliza mahubiri mengi ya ukweli, na wamepitia kazi nyingi ya Mungu. Ilhali kwenye uingiliaji kati na uzuiaji wa mambo mengi tofauti na hali, watu wengi hawawezi kufikia hali ya kutia ukweli katika matendo, na hawawezi kufikia hali ya kumtosheleza Mungu. Watu wanazidi kuwa goigoi, wanazidi kuikosa imani. Wanazidi kuhisi ni kana kwamba matokeo yao binafsi hayajulikani. Hawathubutu kuwa na mawazo yoyote ya kupita kiasi, na hawatafuti kupiga hatua yoyote ya maendeleo; wanafuata tu shingo upande, wakienda mbele hatua kwa hatua. Kuhusiana na hali ya sasa ya binadamu, mwelekeo wa Mungu kwa binadamu ni upi? Tamanio tu la Mungu ni kuukabidhi ukweli huu kwa binadamu, na kutia moyoni mwa binadamu njia Yake, na kupangilia hali mbalimbali ili kujaribu binadamu katika njia tofauti. Shabaha yake ni kuweza kuchukua maneno haya, ukweli huu, na kazi Yake, na kusababisha matokeo ambapo binadamu anaweza kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Watu wengi ambao Nimewaona wanalichukua tu neno la Mungu na kuliona kuwa falsafa, kuliona kuwa barua, kuliona kuwa kanuni za kufuatwa. Wanapoendelea na shughuli zao na kuongea au kukabiliwa na majaribio, hawachukulii njia ya Mungu kama njia ambayo wanafaa kuifuata. Hali hii hasa ni kweli wakati watu wanapokabiliwa na majaribio makuu; Sijamwona yeyote ambaye alikuwa anatia katika matendo kwa mwelekeo wa kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Kwa sababu ya hili, mwelekeo wa Mungu kwa binadamu umejaa chuki na chukizo ya kupindukia. Baada ya Mungu kuwapa watu majaribio kadhaa, hata mara mia, bado hawana mwelekeo wazi wa kuonyesha bidii yao—ninataka kumcha Mungu na kujiepusha na maovu! Kwa sababu watu hawana bidii hii, na hawaonyeshi ishara kama hii, mwelekeo wa sasa wa Mungu kwao si kama ule wa hapo nyuma, Alipotoa rehema Yake, akatoa uvumilivu wake, akatoa ustahimilivu na subira yake. Badala yake, Amesikitishwa mno na binadamu. Ni nani aliyesababisha masikitiko haya? Aina hii ya mwelekeo ambao Mungu anao kwa binadamu, unamtegemea nani? Unategemea kila mtu anayemfuata Mungu. Kwenye mkondo wa miaka Yake mingi ya kazi, Mungu ametaja mahitaji mengi kwa binadamu, na kupangilia hali nyingi kwa binadamu. Lakini haijalishi ni vipi binadamu ametenda, na haijalishi ni mwelekeo upi ambao binadamu anao kwa Mungu, binadamu hawezi kutenda kwa njia wazi kulingana na shabaha ya kumcha Mungu na kujiepusha na uovu. Hivyo basi, Nitajumlisha yote haya kwa msemu mmoja, na kuweza kutumia msemu huu kuelezea kila kitu ambacho tumeweza kuzungumzia kuhusiana na ni kwa nini watu hawawezi kutembea kwa njia ya Mungu—mche Mungu na kujiepusha na maovu. Msemu huu ni upi? Msemu huu ni: Mungu humchukulia binadamu kama kifaa cha wokovu Wake, kifaa cha kazi Yake; binadamu humchukulia Mungu kama adui wake, kama tabaini yake. Je, unalielewa suala hili sasa? Kile ambacho ndicho mwelekeo wa binadamu; kile ambacho ndicho mwelekeo wa Mungu; kile ambacho ni uhusiano wa binadamu na Mungu—hivi vyote viko wazi sana sasa. Haijalishi ni kiwango kipi cha mahubiri ambayo mmeyasikiliza, yale mambo ambayo mliyoyatolea muhtasari nyinyi wenyewe—kama vile kuwa mwaminifu kwa Mungu, kumtii

Mungu, kutafuta njia ya uwiano na Mungu, kutaka kuishi daima dawamu kwa ajili ya Mungu, kuishi kwa ajili ya Mungu—kwangu Mimi mambo hayo hayajumuishi kutembea kwa njia ya Mungu kwa nadhari, ambako ni kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Badala yake, ni njia mbalimbali kupitia kwazo mnaweza kufikia shabaha fulani. Ili kutimiza shabaha hizi, mnaangalia shingo upande baadhi ya taratibu. Na ni taratibu hizi hasa ambazo huwapeleka watu mbali zaidi kutoka katika njia ile ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, na kumweka Mungu katika upinzani na binadamu kwa mara nyingine.

Swali tunalolizungumzia leo ni zito kidogo, lakini licha ya chochote bado Natumai kwamba mtakapopitia yale yote yajayo, na kwenye nyakati zijazo, mnaweza kufanya kile ambacho Nimewaambia mfanye. Msipuuze Mungu na kumchukulia Yeye kama hewa tupu, kuhisi kwamba Anakuwepo tu nyakati zile Anapokuwa Mwenye manufaa kwako, lakini wakati ule ambao humhitaji unahisi kwamba Yeye hayupo. Unaposhikilia uelewa huu katika bila ufahamu, tayari umemghadhabisha Mungu. Pengine kuna watu wanaosema: “Mimi sichukulii Mungu kama hewa tupu, mimi siku zote humwomba Mungu, siku zote mimi humtosheleza Mungu, na kila kitu ninachokifanya huwa katika ule upana na kiwango na kanuni zinazohitajika na Mungu. Bila shaka siendelei kulingana na mawazo yangu binafsi.” Ndiyo, namna ambayo unafanya mambo ni sahihi. Lakini unafikiria vipi wakati unakumbana macho kwa macho na suala? Unakuwa na matendo gani unapokabiliwa na suala? Baadhi ya watu huhisi kwamba Mungu yupo wakati wanapomwomba Yeye, na Kumsihi kuwasikiliza. Lakini wakati wanapokabiliwa na suala wanakuja na fikira zao binafsi na wanataka kuzitii. Hapa Mungu huchukuliwa kama hewa tupu. Aina hii ya hali humfanya Mungu kutokuwepo. Watu hufikiria kwamba Mungu anafaa kuwepo wakati wanapomhitaji Yeye, na wakati hawamhitaji Mungu Hafai kuwepo. Watu hufikiria kwamba kufanya mambo kulingana na mawazo yao katika matendo ya maisha ni tosha. Wanasadiki wanaweza kufanya mambo vyovyote vile wapendavyo. Wanafikiria tu kwamba hawahitaji kutafuta njia ya Mungu. Watu ambao kwa sasa wamo katika aina hii ya hali, hali hii ya namna—huoni kwamba karibu wataingia hatarini? Baadhi ya watu husema: “Haijalishi kama karibu nitaingia hatarini au la, nimesadiki kwa miaka mingi sana, na ninasadiki kwamba Mungu hataniacha kwa sababu Asingeweza kustahimili kuniacha mimi.” Watu wengine husema: “Hata tangu nilipokuwa kwenye tumbo la mama yangu, nilimsadiki Bwana, tangu hapo mpaka sasa, jumla ya miaka arubaini au hamsini hivi. Kwa mujibu wa muda, mimi ndimi nimefuzu zaidi kuokolewa na Mungu; mimi ndimi nimefuzu zaidi kuwepo. Kwenye kipindi hiki cha muda cha miongo minne au mitano, niliacha familia yangu na kazi yangu. Nilijitolea kila kitu nilichokuwa nacho kwa Mungu, kama pesa, ardhi, anasa na muda wa familia; sijala vyakula vingi vitamu; sijafurahia vitu vingi vya kuisisimua; sijatembelea sehemu nyingi za kuvutia; nimeweza hata kupitia mateso ambayo hata watu wa kawaida wasingevumilia. Kama Mungu hawezi kuniokoa

mimi kwa sababu ya haya yote, basi mimi nashughulikiwa kwa njia isiyo ya haki na siwezi kuamini kwa aina hii ya Mungu.” Je, kunao watu wengi walio na aina hii ya mtazamo? (Kunao wengi sana.) Basi leo Nitawasaidia kuelewa hoja moja: Kila mmoja wa hao anayeshikilia aina hii ya maoni anachukua hatua zitakazomdhuru mwenyewe. Hii ni kwa sababu wanatumia maoni yao binafsi katika kuyafunika macho yao. Ni kufikiria kwao hasa, na hitimisho yao binafsi zinazochukua nafasi ya kiwango cha kile Mungu anahitaji kutoka kwa binadamu, ndizo zinazowashikilia dhidi ya kukubali nia za kweli za Mungu, na kuwafanya kutoweza kuhisi uwepo wa kweli wa Mungu, na kuwafanya pia kupoteza fursa yao kufanywa kuwa watimilifu na Mungu na kutokuwa na sehemu au mgao katika ahadi ya Mungu.

Namna Ambavyo Mungu Huanzisha Matokeo Ya Binadamu na Kiwango Ambacho Hutumia Kuasisi Matokeo ya Binadamu

Kabla ya kuwa na mitazamo au hitimisho zako binafsi, unafaa kwanza kuelewa mwelekeo wa Mungu kwako, kile ambacho Mungu anafikiria, na kuamua kama kufikiria kwako ni sahihi au la. Mungu hajawahi kutumia vipimo vya muda katika kuasisi matokeo ya mtu, na Hajawahi kutumia kiwango cha mateso yaliyovumiliwa na mtu katika kuasisi matokeo yake. Basi Mungu hutumia kiwango gani katika kuasisi matokeo ya binadamu? Kutumia vipimo vya muda katika kuasisi matokeo ya binadamu—hii ndiyo inaingiliana zaidi na dhana za watu. Na pia kuna hao watu binafsi ambao mara nyingi mnawaona, wale ambao katika wakati fulani walijitolea kabisa, watumia muda mwingi kabisa, wakagharamika kabisa, wakateseka kabisa. Hawa ndio, kwa maoni yenu, wanaweza kuokolewa na Mungu. Kile tu ambacho watu hawa wanaonyesha, yote wanayoishi kwa kudhihirisha, ndiyo hasa dhana ya wanadamu kuhusu kiwango ambacho Mungu anaanzisha kuhusiana na matokeo ya binadamu. Bila kujali ni nini unachosadiki, Sitaorodhesha mifano hii mmoja baada ya mwingine. Nikiongea kwa ujumla, mradi tu si kiwango cha kufikiria binafsi kwa Mungu, basi kinakuja kutoka kwenye kufikiria kwa binadamu na ni dhana tu ya binadamu. Ni nini athari za kusisitiza bila mwelekeo dhana na kufikiria kwako binafsi? Bila shaka, athari inaweza kuwa tu Mungu akikusukuma mbali. Hii ni kwa sababu siku zote unaringa kuhusu sifa zako mbele ya Mungu, unashindana na Mungu, na kuleta mzozo dhidi ya Mungu, na hujaribu hata kufahamu kwa kweli kufikiria kwa Mungu, wala hujaribu kuzifahamu nia za Mungu na mwelekeo wa Mungu kwa binadamu. Kuendelea mbele hivi ni kujiheshimu kuliko yote na wala si kumheshimu Mungu. Unajisadiki; husadiki Mungu. Mungu hataki mtu wa aina hii, na Mungu hatamwokoza mtu wa aina hii. Kama huwezi kuachilia aina hii ya mtazamo, na kisha kuirekebisha mitazamo hii ya kale isiyokuwa sahihi; kama ungeweza kuendelea mbele kulingana na maagizo ya Mungu; anza kutenda njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu kwa sasa na kusonga mbele; kuweza kuheshimu Mungu na kumwona kuwa mkubwa katika mambo yote; usitumie ndoto zako za kibinafsi, mitazamo au imani katika kujifafanua,

kumfafanua Mungu. Na badala yake, unazitafuta nia za Mungu kwa hali zote, unatimiza utambuzi na uelewa wa mwelekeo wa Mungu kwa binadamu, na unatumia kiwango cha Mungu kutosheleza Mungu—kufanya hivi kungependeza! Huku kungemaanisha karibu unaanza katika njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu.

Kwa sababu Mungu hatumii namna ambavyo watu hufikiria kwa njia hii au njia ile mawazo na mitazamo yao, kama kiwango cha kuanzisha matokeo ya binadamu, basi ni aina ipi ya kiwango Anayoitumia? Mungu hutumia majaribio kuanzisha matokeo ya binadamu. Kunavyo viwango viwili vya kutumia katika majaribio yanayoasisi matokeo ya binadamu: Kiwango cha kwanza ni idadi ya majaribio ambayo watu hao wanapitia, na kiwango cha pili ni matokeo ya watu hawa katika majaribu haya. Ni viashirio hivi viwili vinavyoasisi matokeo ya binadamu. Sasa tutaweza kufafanua viwango hivi viwili.

Kwanza kabisa, unapokabiliwa na jaribio kutoka kwa Mungu (kidokezo: Inawezekana kwamba katika macho yako jaribio hili ni dogo sana na halifai kutajwa), Mungu atakufanya kuwa na ufahamu kabisa kwamba huu ni mkono wa Mungu juu yako, na kwamba ni Mungu ambaye amepangilia hali hizi zote kwako. Wakati kimo chako hakijakomaa, Mungu atapanga majaribio ili kuweza kukupima. Majaribio haya yatalingana na kimo chako, yale ambayo unaweza kuelewa, na yale ambayo unaweza kustahimili. Kujaribu sehemu yako gani? Kujaribu mwelekeo wako kwa Mungu. Je, mwelekeo huu ni muhimu sana? Bila shaka ni muhimu! Zaidi ya hayo, ni muhimu hasa! Kwa sababu mwelekeo huu wa binadamu ndiyo matokeo anayotaka Mungu, ndicho kitu muhimu zaidi kulingana na Mungu. Ama sivyo Mungu asingetumia jitihada Zake kwa watu kwa kujihusisha na aina hizi za kazi. Mungu hutaka kuuona mwelekeo wako kwake Yeye, kupitia kwa majaribio haya; Anataka kujua kama uko kwenye njia sahihi na Anataka kujua kama unamcha Mungu na kujiepusha na maovu. Hivyo basi, bila kujali kama unaelewa ukweli mwingi au kidogo wakati huo, bado utakabiliwa na majaribio ya Mungu, na kufuatia ongezeko lolote katika kiwango chochote cha ukweli unaouelewa, Mungu ataendelea kupangilia majaribio sawa na hayo kwako. Wakati unapokabiliwa kwa mara nyingine tena na jaribio, Mungu anataka kuona iwapo mtazamo wako, mawazo yako, na mwelekeo wako kwa Mungu umekuwa na ukuaji wowote mpaka sasa. Baadhi ya watu husema: “Kwa nini siku zote Mungu anataka kuiona mielekeo ya watu? Kwani Mungu hajaona namna wanavyoweza ukweli katika matendo? Kwa nini Atake tena kuiona mielekeo ya watu?” Huku ni kupayuka kwa upuuzi! Kwa sababu Mungu anaendelea hivi, basi nia za Mungu lazima ziwe mumohumo. Siku zote Mungu huwaangalia watu kutoka pembeni mwao, akiangalia kila neno na tendo lao, kila kitendo na kusonga kwao, na hata kila fikira na wazo lao. Kila kitu kinachowafanyikia watu: vitendo vyao vizuri, makosa yao, dhambi zao, na hata kuasi na kusaliti kwao, Mungu atazirekodi zote kama ithibati katika kuasisi matokeo yao. Kwa kadri kazi ya Mungu inavyoendelea

kuimarika hatua kwa hatua, unasikia ukweli zaidi na zaidi, unakubali mambo mazuri zaidi na zaidi, taarifa nzuri, na uhalisia wa kweli. Kwenye mkondo wa mchakato huu, mahitaji ya Mungu kwako wewe yataongezeka pia. Wakati uo huo, Mungu atapanga majaribio makubwa zaidi kwako. Shabaha yake ni kuchunguza kama mwelekeo wako kwa Mungu umekomaa mpaka sasa. Bila shaka, kwenye kipindi hiki, mtazamo ambao Mungu anahitaji kwako unaingiliana na uelewa wako wa uhalisia wako wa ukweli.

Huku kimo chako kinapoendelea kuimarika kwa utaratibu, kile kiwango ambacho Mungu anahitaji kutoka kwako wewe kitaendelea kuimarika kwa utaratibu pia. Kama utakuwa hujakomaa, Mungu atakupa kiwango kidogo sana; wakati kimo chako kitakapokuwa kikubwa kidogo, Mungu atakupa kiwango cha juu zaidi kidogo. Lakini Mungu atakuwa vipi baada ya wewe kuuelewa ukweli wote? Mungu atahakikisha kuwa unakabiliana na hata majaribio makubwa zaidi. Katikati ya majaribio haya, kile Mungu anachotaka kupata, kile Mungu anachotaka kuona, ni maarifa yako ya kina zaidi ya Mungu na kumcha kwako Kwake kwa njia ya kweli. Wakati huu, mahitaji ya Mungu kwako wewe yatakuwa ya juu zaidi “makali zaidi” kuliko wakati ambapo kimo chako kilikuwa kidogo zaidi (kidokezo: Watu huona kwamba hali hii ni kali, lakini Mungu kwa hakika Huiona kuwa ya kustahimilika). Wakati Mungu anawapa watu majaribio, ni uhalisia gani ambao Mungu anataka kuunda? Mungu anauliza kila mara kwamba watu wampe Yeye moyo wao. Baadhi ya watu watasema: “Mtu anawezaje kufanya hivyo? Natekeleza wajibu wangu, niliacha nyumba yangu na riziki yangu, niligharamika kwa sababu ya Mungu. Hii yote si mifano ya kuutoa moyo wangu kwa Mungu? Ni vipi vingine nitakavyutoa moyo wangu kwa Mungu? Yaweza kuwa kwamba, hii si mifano ya kuutoa moyo wangu kwa Mungu? Mahitaji mahususi ya Mungu ni yapi?” Mahitaji haya ni mepesi mno. Kwa hakika, kunao baadhi ya watu ambao tayari wameitoa mioyo yao kwa Mungu katika viwango tofauti na awamu mbalimbali za majaribio yao. Lakini wengi wa watu huwa hawapi Mungu mioyo yao. Wakati Mungu anapokupa jaribio, Mungu hutaka kujua kama moyo wako uko pamoja Naye, pamoja na mwili au pamoja na Shetani. Wakati Mungu anapokupa jaribio, Mungu anataka kujua kama unasimama katika upinzani na Yeye au kama unasimama katika hali ambayo inalingana na Yeye, na kutaka kuona moyo wako kama uko na Yeye. Wakati hujakomaa na wakati wa kukabiliwa na majaribio, kiwango cha imani yako kiko chini, na huwezi kujua hasa ni nini unachohitaji ili kutosheleza nia za Mungu kwa sababu unao uelewa finyu wa ukweli. Licha ya haya yote, bado unaweza kumwomba Mungu kwa dhati na uaminifu, kuwa radhi kuutoa moyo wako kwa Mungu, kumfanya Mungu kuwa mkuu wako, na kuwa radhi kumpa Mungu yale mambo unayosadiki kuwa yenye thamani zaidi. Hii ndiyo maana ya wewe kuwa tayari umempa Mungu moyo wako. Unaposikiliza mahubiri mengi zaidi na zaidi, na kuelewa ukweli zaidi na zaidi kimo chako kitaanza kukomaa kwa utaratibu. Kiwango ambacho Mungu huhitaji kutoka

kwako si sawa na kile ambacho ulikuwemo wakati ulikuwa hujakomaa; Anahitaji kiwango cha juu zaidi kuliko hicho. Wakati moyo wa binadamu unapewa Mungu kwa utaratibu, unaanza kuwa karibu zaidi na karibu zaidi na Mungu; wakati binadamu anaweza kuwa karibu na Mungu kweli, wanaanza kuwa na moyo ambao sanasana unamcha Yeye. Mungu anataka aina hii ya moyo.

Wakati Mungu anataka kuumiliki moyo wa mtu, Atawapa majaribio mengi. Kwenye majaribio haya, kama Mungu hatachukua moyo wa mtu huyu, wala Haoni kama mtu huyu anao mwelekeo wowote—hivi ni kusema Havioni vitu ambavyo mtu huyu anapitia au anafanya mambo kwa njia ambayo ni ya kumcha Mungu, na Haoni mwelekeo au suluhisho ambalo linajiepusha na maovu kutoka kwa mtu huyu. Kama hivi ndivyo ilivyo, basi baada ya majaribio mengi, subira ya Mungu kwa mtu huyu binafsi itaondolewa, na Hatamvumilia mtu huyu tena. Hataweza kuwapa watu kama hawa majaribio, na Hataweza tena kuwashughulikia. Basi hiyo inamaanisha nini kwa matokeo ya mtu huyu? Inamaanisha kwamba hawatakuwa na matokeo. Yawezekana kwamba mtu huyu hajafanya maovu yoyote. Yawezekana pia kwamba watu hawa hawajafanya chochote cha kukatiza au kutatiza. Yawezekana kuwa watu hawa hawajampinga Mungu waziwazi. Hata hivyo, moyo wa mtu huyu umefichwa kutoka kwa Mungu. Hawajawahi kuwa na mwelekeo na mtazamo wazi kwa Mungu, na Mungu hawezi kuona waziwazi kwamba moyo wake amekabidhiwa Yeye, na Yeye Hawezi kuona waziwazi kwamba mtu huyu anatafuta kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Mungu hana subira tena kwa watu hawa, Hatawagharamia tena, Hatatoa tena rehema Yake kwao, na Hatawafanyia kazi wao tena. Maisha ya imani ya mtu huyu katika Mungu tayari hayapo tena. Hii ni kwa sababu katika majaribio yote mengi ambayo Mungu amempa mtu huyu, Mungu hajapata matokeo Anayotaka. Hivyo basi, kunayo idadi ya watu ambao ndani yao Sijawahi kuuona mwangaza na kupata nuru kwa Roho Mtakatifu. Inawezekanaje kuona haya? Mtu wa aina hii huenda aliamini katika Mungu kwa miaka mingi, na kwenye sehemu ya juujuu wamekuwa amilifu. Wamevisoma vitabu vingi, wameyashughulikia masuala mengi, wameandika nakala nyingi, wamekuwa na ujuzi wa barua na falsafa nyingi. Hata hivyo, hakuna ukuaji wowote unaonekana kamwe, na wala kuwa na mtazamo wowote wa kuonekana kwa Mungu kutoka kwa mtu huyu, wala hakuna mwelekeo wowote wazi. Hivi ni kusema kwamba huwezi kuona moyo wa mtu huyu. Moyo wao siku zote umesetiriwa, moyo wao umefumikwa—Umefunikwa kutoka kwa Mungu, hivyo basi Mungu hajauona moyo wa kweli wa mtu huyu, Hajaona kumcha Mungu kwa mtu huyu, na hata zaidi Hajaona namna ambayo mtu huyu anatembea katika njia za Mungu. Kama mpaka sasa Mungu hajampata mtu wa aina hii, Anaweza kuwapata katika siku za usoni? Hawezi! Je, Mungu ataendelea kusukumiza mbele mambo ambayo hayawezi kupatikana? Hatafanya hivyo! Mwelekeo wa Mungu kwa watu kama hawa, hivyo basi ni nini? (Anawasukumia mbali,

Hawasikilizi.) Yeye hawasikilizi! Mungu hasikilizi mtu wa aina hii; Anawasukumia mbali. Mmetia kwenye kumbukumbu maneno haya kwa haraka sana, kwa usahihi sana. Inaonekana mmelewa kile mlichosikia!

Kunao baadhi ya watu ambao, punde wanapoanza kumfuata Mungu wao hawana ukomavu na hawajui chochote; hawaelewi nia za Mungu; hawajui pia maana ya kusadiki Mungu, kuchukua njia iliyoundwa na binadamu na inayokosewa na wengi ya kusadiki Mungu, kufuata Mungu. Wakati mtu wa aina hii anakabiliwa na majaribio hawana habari na hawajali kuhusu mwongozo na nuru ya Mungu. Hawajui maana ya kuutoa moyo wao kwa Mungu na maana ya kusimama imara wakati wa jaribio. Mungu atampa mtu huyu kiwango finyu cha muda na katika kipindi hiki, Atawaacha kuelewa jaribio la Mungu ni nini, na nia za Mungu ni nini. Baadaye mtu huyu atahitaji kuonyesha mtazamo wao. Kuhusiana na watu wale walio katika awamu hii, Mungu angali anasubiri. Kuhusiana na watu wale ambao mitazamo yao ingali inayumbayumba, wale wanaotaka kumpa Mungu mioyo yao lakini hawajawa na maridhiano ya kufanya hivyo, ambao, ingawa wameweza kutenda ukweli fulani, wakati wanapokumbwa na jaribio kuu, wanaokwepa na wanataka kukata tamaa—mwelekeo wa Mungu kwa watu kama hawa ni upi? Mungu angali bado ana matarajio kidogo kwa watu kama hawa. Matokeo yanategemea na mielekeo na utendakazi wao. Mungu anaitikia vipi kama watu si amilifu katika kuwa na maendeleo? Yeye hukata tamaa. Hii ni kwa sababu kabla Mungu hajakata tamaa kwako, tayari wewe mwenyewe umekata tamaa. Kwa hivyo, huwezi kumlaumu Mungu kwa kufanya hivyo, je, unaweza? Je, hiyo ni haki? (Ni haki.)

Swali la Kiutendaji Huleta Aina Zote za Aibu kwa Watu

Kunayo aina nyingine ya mtu aliye na matokeo mabaya zaidi kati ya yote. Hawa ndio Nisiopenda kutaja sana. Hali si mbaya kwa sababu mtu huyu hupokea adhabu ya Mungu, au kwamba mahitaji ya Mungu kwao ni makali na wana matokeo mabaya. Badala yake, hali ni mbaya kwa sababu wanajifanyia wenyewe, kama inavyosemwa mara kwa mara: Wanajichimbia kaburi lao. Mtu kama huyu ni aina gani? Mtu huyu hatembezi kwenye njia inayofaa, na matokeo yake yanafichuliwa mapema. Mungu humwona mtu wa aina hii kama lengo Lake kubwa zaidi la chuki Yake. Kama watu wanavyosema hawa ndio wa huzuni kuliko wote. Mtu wa aina hii ni mwenye shauku anapoanza kumfuata Mungu; wanalipia bei nyingi; wanayo maoni mazuri kuhusu mtazamo wa kazi ya Mungu; kufikiria kwao ni kwingi kuhusu mustakabali wao binafsi; wao hasa wanayo imani katika Mungu, wanasadiki kwamba Mungu anaweza kumfanya binadamu kuwa kamili, na kumfanya huyo binadamu kufikia hatima yenye utukufu. Ilhali kwa sababu isiyoeleweka, mtu huyu kisha hukimbia akiwa katika harakati ya kazi ya Mungu. Ni nini maana ya mtu huyu kukimbia? Maana yake ni kwamba wanatoweka bila kwaheri, bila sauti

yoyote. Wanaondoka bila kutaja neno lolote. Ingawa mtu wa aina hii anadai kuwa anasadiki Mungu, huwa haweki kamwe mizizi yoyote kwenye njia ya kusadiki Mungu. Hivyo basi, haijalishi ni kwa muda upi wamesadikia, bado wanaweza kumgeuka Mungu. Baadhi ya watu huondoka ili kufanya biashara, baadhi ya watu huondoka ili kuishi maisha yao, baadhi ya watu huondoka ili kutajirika, baadhi ya watu huondoka kuoa au kuolewa, kuwa na watoto.... Miongoni mwa wale wanaondoka, kuna wanaopata shambulizi la nadhari na wanataka kurudi, na wengine wanaoendelea vibaya sana kimaisha, wanaishi maisha tu na kuyasukuma kwa miaka na miaka. Wasukuma maisha hawa wamepitia mateso mengi, na wanasadiki kwamba kuwa ulimwenguni kuna maumivu mno, na hawawezi kutenganishwa na Mungu. Wanataka kurudi nyumba ya Mungu ili kupokea tulizo, amani, furaha, na kuendelea kusadiki katika Mungu ili kukwepa janga, au kuokolewa na kupata hatima nzuri. Hii ni kwa sababu watu hawa wanasadiki kwamba upendo wa Mungu hauna mipaka, kwamba neema ya Mungu haiwezi kuisha na kwamba haiwezi kutumika yote. Wanasadiki kwamba haijalishi ni nini mtu amefanya, Mungu anafaa kumsamehe na kuvumilia maisha yao ya kale. Watu hawa wanasema mara kwa mara ya kwamba wanataka kurudi na kufanya wajibu wao. Kuna wale ambao hata hupa baadhi ya mali yao kanisa, wakitumai kwamba hii ndiyo njia yao ya kurudi katika nyumba ya Mungu. Mwelekeo wa Mungu kwa watu aina hii ni upi? Mungu anafaa kuanzisha vipi matokeo yao? Kuwa huru kuongea. (Ulifikiri kwamba Mungu angewakaribisha watu wa aina hii, lakini baada ya kusikia kwamba sasa hivi, pengine hawatakaribishwa tena.) Na wewe unafikiria vipi? (Mtu wa aina hii huja mbele ya Mungu ili matokeo yao yasije yakawa yale ya kifo. Hawafanyi hivyo kutokana na uaminifu wa kweli. Badala yake, kutokana na maarifa kwamba kazi ya Mungu itakamilika hivi karibuni, wanadanganyika kuwa watapata baraka.) Unasema kwamba mtu huyu kwa kweli hasadiki katika Mungu, na hivyo basi Mungu hawezi kumkubali? Ndivyo ilivyo? (Ndiyo.) (Uelewa wangu ni kwamba mtu wa aina hii ni yule wa kujali maslahi yake kuliko uhaki wa jambo, na kwamba hamsadiki Mungu kwa dhati.) Hajapata kumsadiki Mungu; yeye ni mtu mwenye kuangalia maslahi yake kuliko haki. Yamesemwa vizuri! Watu hawa wanaojali maslahi yao ni wale ambao kila mmoja anawachukia. Wanaenda na mkondo tu, na hawawezi kusumbuliwa ili kufanya kitu isipokuwa kama watafaidi kwa jambo hilo. Bila shaka wanastahili dharau! Je, kati ya ndugu zangu wengine kunaye anayo maoni? (Mungu hatawakubali tena kwa sababu kazi ya Mungu karibu inakamilika na sasa ndipo matokeo ya watu yanaandaliwa. Ni wakati huu ambapo watu hawa wanataka kurudi. Si kwa sababu kwa kweli wanataka kufuata ukweli; wanataka kurudi kwa sababu wanayaona majanga yakishushwa, au wanashawishiwa na mambo ya nje. Kama kweli walikuwa na moyo uliokuwa ukifuatilia ukweli, wasingewahi kukimbia wakiwa katikati ya safari.) Je, yapo maoni mengine? (Hawatakubaliwa. Kwa kweli Mungu aliwapa fursa lakini mwelekeo wao kwake Mungu ulikuwa siku zote kutomsikiliza. Bila kujali nia za mtu huyu ni zipi, na hata kama atatubu, Mungu bado hatamkubali. Hii ni kwa

sababu Mungu tayari aliwapa fursa nyingi ajabu ilhali wao walionyesha mtazamo wao: Walitaka kumwacha Mungu. Hivyo basi, watakaporudi sasa, Mungu hatawakaribisha.) (Ninakubali pia kwamba Mungu hatamkaribisha mtu wa aina hii, kwa sababu kama mtu ameona njia ya kweli, akapitia kazi ya Mungu kwa kipindi kirefu kama hicho, na bado anaweza kurudi kwa ulimwengu, kurudi kwa kumbatio la Shetani, basi huu ni usaliti mkuu kwa Mungu. Licha ya hoja kwamba kiini cha Mungu ni rehema, ni upendo, inategemea ni mtu wa aina gani ambaye kiini hicho kinaelekezwa kwake. Kama mtu huyu atakuja mbele ya Mungu akitafuta faraja, kitu cha kuwekea tumaini lake, basi mtu wa aina hii kwa kweli si mtu anayemsadiki Mungu kwa dhati, na rehema za Mungu kwake zinafika hapo.) Kiini halisi cha Mungu ni rehema, kwa hivyo ni kwa nini Hampatii mtu wa aina hii rehema zaidi kidogo tu? Kwa rehema kidogo, hawapati fursa? Awali, mara nyingi ilisemekana: Mungu anamtaka kila mmoja kuokolewa, na hataki mtu yeyote kuangamia. Kama kondoo mmoja miongoni mwa kondoo mia moja atapotea, Mungu atawaacha wale kondoo tisini na tisa kumtafuta yule kondoo aliyepotea. Siku hizi, kuhusiana na mtu wa aina hii, kama ni kwa minajili ya kusadiki kwao kwa Mungu, je, Mungu anafaa kuwakaribisha na kuwapa fursa ya pili? Kwa kweli hilo si swali gumu; ni rahisi mno! Kama kwa kweli mnamtambua Mungu na mnao uelewa halisi wa Mungu, basi hamna ufafanuzi mwingi unaohitajika; hamna kukisia kwingi kunahitajika vilevile, kweli? Majibu yenu yamo katika njia sahihi, lakini bado upo umbali fulani kati yao na mwelekeo wa Mungu.

Sasa hivi tu kulikuwepo na baadhi yenu mliokuwa na hakika kwamba Mungu asingeweza kumkubali mtu wa aina hii. Wengine hawakuwa na hakika sana kuwa Mungu anaweza kuwakubali, na huenda asiwakubali—mwelekeo huu ndio ule wa wastani; na kisha kulikuwa na wale ambao mtazamo wao ulikuwa kwamba wanatumai kwamba Mungu atamkaribisha mtu wa aina hii—huu ndio mwelekeo ule usioeleweka. Wale walio na mwelekeo hakika wanasadiki kuwa Mungu ameshughulika mpaka sasa, na shughuli Yake imekamilika, hivyo basi Mungu hahitaji kuwa mvumilivu na watu hawa, na kwamba Hatawakaribisha tena. Wale watu wa wastani wanasadiki kwamba masuala haya yanafaa kushughulikiwa kulingana na hali inayoyazunguka: Kama moyo wa mtu huyu hauwezi kutenganishwa na wa Mungu, na bado wao ni watu wanaomsadiki Mungu kwa kweli, mtu anayefuatilia ukweli, basi Mungu hafai kukumbuka udhaifu na makosa yao ya awali; Anafaa kuwasamehe, na kuwapa fursa nyingine, kuwaruhusu kurudi katika nyumba ya Mungu, na kukubali wokovu wa Mungu. Hata hivyo, kama mtu huyu atatoroka kwa mara nyingine, hapo ndipo Mungu hatataka mtu huyu na kitendo hiki hakitachukuliwa kuwa cha ukiukaji wa haki. Kunalo kundi jingine ambalo linatumaini kwamba Mungu anaweza kumkaribisha mtu huyu. Kundi hili halina uhakika sana kama Mungu anawakaribisha au la. Kama wanaamini kwamba Mungu anafaa kuwakaribisha, lakini Mungu asiwakaribishe, basi yaonekana kwamba wamepotoka kidogo na mtazamo wa Mungu. Kama

watasadiki kwamba Mungu hafai kuwakaribisha, naye Mungu atokee kusema kwamba upendo Wake kwa binadamu hauna kikomo na kwamba Yuko radhi kumpa mtu fursa nyingine, basi huu si mfano wa kutojua kwa binadamu ukimulikwa waziwazi? Kwa vyovyote vile, nyinyi nyote mna mitazamo yenu binafsi. Mitazamo hii ni maarifa katika fikira zenu binafsi; ni onyesho pia ya kina cha uelewa wenu wa kweli na uelewa wenu wa nia za Mungu. Imesemwa vyema, sio? Ni jambo la kupendeza kwamba mnayo maoni katika suala hili! Lakini suala kuhusu kama maoni yenu ni sahihi au si sahihi, kunayo alama ya kiulizo. Je, nyinyi nyote hamna wasiwasi kidogo? “Basi ni gani sahihi? Siwezi kuona vizuri, na sijui hasa kile anachofikiria Mungu. Mungu hakuniambia chochote. Naweza kujua anachofikiria Mungu? Mtazamo wa Mungu kwake binadamu ni upendo. Kulingana na mwelekeo wa kale wa Mungu, Anafaa kumkubali mtu huyu. Lakini sina hakika kuhusu mwelekeo wa sasa wa Mungu—ninaweza kusema tu kwamba pengine Atamkaribisha mtu huyu na pengine Hatamkaribisha.” Je, waona vile jambo hili lilivyo la mzaha? Jambo hili limewakoroga. Kama hamna msimamo bora wa suala hili basi ni nini mtakachofanya endapo kanisa lenu litakumbana kwa kweli na mtu wa aina hii? Kama hamtalishughulikia kwa njia bora, basi pengine mtamkosea Mungu. Je, hamuoni kwamba suala hili ni hatari mno?

Kwa nini Ninataka kuulizia maoni yenu kuhusu kile Nilichokuwa Nazungumzia? Nataka kupima mitazamo yenu, kupima ni maarifa kiasi kipi ya Mungu mliyo nayo, ni uelewa kiasi kipi mlilo nao katika nia za Mungu na mwelekeo wa Mungu. Jibu ni gani? Jibu limo kwenye mitazamo yenu. Baadhi yenu mnashikilia sana ukale, na baadhi yenu mnatumia kufikiria kwenu katika kukisia. “Kukisia” ni nini? Ni wakati ule ambao hamna wazo lolote namna ambavyo Mungu anafikiria, hivyo basi mnakuja na mawazo yasiyo na msingi kuhusu namna ambavyo Mungu anafaa kufikiria kwa namna hii au namna ile. Hamjui kwa hakika kama kukisia kwenu ni sahihi au si sahihi, na hivyo basi mnatoa mtazamo usioleweka. Mkikumbwa na hoja hii mnaona nini? Wakati wakimfuata Mungu, ni nadra sana kwa watu kutilia maanani makusudi ya Mungu, na ni nadra wao kutilia maanani mawazo ya Mungu na mtazamo Wake kwa wanadamu. Watu hawaelewi fikira za Mungu, kwa hivyo mnapoulizwa maswali yanayohusisha nia za Mungu, yanayohusisha tabia ya Mungu, mnaingia katika hali ya kutokuwa na hakika; mnakuwa kwa kweli hamna uhakika, na mnakisia au kubahatisha. Mwelekeo huu ni upi? Unathibitisha hoja hii: kwamba watu wengi wanaomwamini Mungu wanamchukulia kuwa kifungo cha hewa tupu na kama kitu kinachoonekana kuishi dakika moja na hakipo tena dakika ifuatayo. Kwa nini Nasema hivyo? Kwa sababu kila wakati mnapokumbwa na suala, hamzijui nia za Mungu. Kwa nini hamzijui? Si kwamba hamzijui tu kwa sasa. Badala yake kuanzia mwanzo hadi mwisho hamjui mwelekeo wa Mungu katika suala hili. Kwenye nyakati zile ambazo huwezi kuona na hujui mwelekeo wa Mungu, umewahi kuutafakaria? Umeutafuta? Umewasiliana ili kuupata? La! Hii

inathibitisha hoja: Mungu unayemsadiki na Mungu wa kweli hawajaunganika. Wewe, unayemsadiki Mungu, unafikiria Mungu kuhusu mapenzi yako, unafikiria tu kuhusu mapenzi ya kiongozi wako, na unafikiria tu yale mambo ya juujuu na maana ya kifalsafa ya neno la Mungu, lakini hujaribu kwa kweli kujua na kutafuta mapenzi ya Mungu kamwe. Sivyo ndivyo hali ilivyo? Kiini halisi cha suala hili hakipendezi! Kwa miaka na mikaka Nimeona watu wanaomsadiki Mungu. Kusadiki huku kunachukua mfumo gani? Baadhi ya watu wanasadiki katika Mungu ni kana kwamba Yeye ni hewa tupu. Watu hawa hawana majibu ya maswali kuhusu uwepo wa Mungu kwa sababu hawawezi kuhisi au kuwa na ufahamu uwepo au kutokuwepo kwa Mungu, sikuambii hata kuuona waziwazi au kuuelewa. Kwa nadharia yao, watu hawa wanafikiria kwamba Mungu hayupo. Baadhi wanasadiki katika Mungu ni kana kwamba Yeye ni binadamu. Watu hawa wanasadiki kwamba Mungu hawezi kufanya mambo yale ambayo wao hawawezi kufanya, na kwamba Mungu anafaa kufikiria namna wanavyofikiria. Ufafanuzi wa mtu huyu kuhusu Mungu ni “mtu asiyeonekana na asiyegusika.” Kunalo pia kundi la watu wanaosadiki katika Mungu kana kwamba Yeye ni kikaragosi; watu hawa wanasadiki kwamba Mungu hana hisia. Wanafikiria kwamba Mungu ni sanamu ya matope, na kwamba wanapokabiliwa na jambo, Mungu hana mwelekeo, hana mtazamo, hana mawazo; Anatawaliwa na binadamu. Watu wanasadiki tu wanavyotaka kusadiki. Wakimfanya kuwa mkubwa, Yeye ni mkubwa; wakimfanya kuwa mdogo, Yeye ni mdogo. Wakati wanapotenda dhambi na wanahitaji rehema ya Mungu, wanahitaji uvumilivu wa Mungu, wanahitaji upendo wa Mungu, basi Mungu anafaa kutoa rehema Zake. Watu hao wanafikiria kuhusu Mungu kwenye akili zao binafsi na kumfanya Mungu kutimiza mahitaji yao na kutosheleza matamania yao yote. Haijalishi ni lini na ni wapi, na haijalishi hata mtu huyu anafanya nini, watakubali mvuto huu katika matendo yao kwa Mungu na kusadiki kwao katika Mungu. Kuna hata wale wanaosadiki katika Mungu kuweza kuwaokoa baada kuikera tabia ya Mungu. Hii ni kwa sababu wanasadiki kuwa upendo wa Mungu hauna mipaka, tabia ya Mungu ni haki, na kwamba bila kujali ni vipi ambavyo watu wanakosea Mungu, Hatakumbuka chochote. Kwa sababu makosa ya binadamu, dhambi za binadamu na kutotii kwa binadamu ni maonyesho ya mara moja ya tabia ya mtu huyo, Mungu atawapatia watu fursa, kuvumilia na kuwa na subira nao. Mungu angali atawapenda kama awali. Kwa hivyo tumaini la wokovu wao lingali kubwa. Kwa hakika, haijalishi ni vipi mtu anavyosadiki Mungu, mradi tu hafuatilii ukweli basi Mungu anashikilia mwelekeo mbaya kwake. Hii ni sababu wakati unamsadiki Mungu, labda unakithamini kile kitabu cha neno la Mungu unakichambua kila siku, unakisoma kila siku, lakini unamweka Mungu halisi pembeni, unamchukulia kama hewa tupu, unamchukulia Yeye kama mtu, na baadhi yenu mnamchukulia kuwa kikaragosi. Kwa nini Nasema hivi? Kwa sababu kutokana na vile Ninavyoona, licha ya kama unakabiliwa na suala au kukumbana na hali, yale mambo yanayopatikana katika nadharia yako, yale mambo ambayo yameimarishwa ndani kwa ndani—hakuna kati ya haya ambayo yana

uunganisho wa neno la Mungu au yanafuatilia ukweli. Unajua tu kile wewe mwenyewe unatafuta, maoni yako wewe binafsi, na kisha mawazo yako binafsi, mitazamo yako binafsi inalazimishiwa Mungu. Inakuwa mitazamo ya Mungu. Akilini mwako hii inakuja kuwa mitazamo ya Mungu, na unafanya hii mitazamo kuwa viwango ambavyo unavishikilia bila kutetereka. Kwa muda, kuendelea namna hii kunakufanya uwe mbali na mbali kutoka kwa Mungu.

Elewa Mwelekeo wa Mungu na Utupilie Mbali Dhana zote Potovu Kumhusu Mungu

Mungu huyu ambaye kwa sasa mnasadiki, mmewahi kufikiria kuhusu Yeye ni Mungu wa aina gani? Anapomwona mtu mwovu akifanya mambo maovu, je Anayachukia? (Anayachukia.) Anapooni makosa ya mtu asiyejua, mwelekeo Wake ni upi? (Huzuni.) Anapowaona watu wakiiba sadaka Yake, mwelekeo Wake ni upi? (Anawachukia.) Haya yote yako wazi, sivyo? Anapooni mtu akiwa mzembe katika kusadiki kwake Mungu, na mtu huyo akikosa kufuatilia ukweli kwa namna yoyote, mwelekeo wa Mungu ni upi? Bado hamjalewa jambo hili, sivyo? Uzembe ni mwelekeo ambao si dhambi, na humkosei Mungu. Watu husadiki kwamba haupaswi kuchukuliwa kama kosa. Basi mnafikiria mwelekeo wa Mungu ni nini? (Hayuko radhi kujibu swali hili.) Hayuko radhi kulijibu—mwelekeo huu ni upi? Ni kwamba Mungu huwa anawadharau watu hawa, anawabeza watu hawa! Mungu hushughulikia watu hawa kwa kutowathamini. Mtazamo wake ni kuwaweka pembeni, kutojikusisha na kazi yoyote inayowahusu, ikiwemo kuwapa nuru, mwangaza, kuwarudi au kuwafundisha nidhamu. Mtu wa aina hii kwa kweli si wa thamani kwa kazi ya Mungu. Mwelekeo wa Mungu kwa watu wanaozikera tabia Yake, na kuzikosea amri Zake za kiutawala ni upi? Chuki mno kwa kupindukia! Kwa kweli Mungu hupandwa na hasira kali na watu ambao hawaghairi kuhusu kukera tabia Yake! “Hasira Kali” ni hisia tu, hali ya moyo; haiwezi kuwakilisha mwelekeo kamili. Lakini hisia hii, hali hii ya moyo, itasababisha matokeo kwa mtu huyu: Itamjaza Mungu na chukizo la kupindukia! Ni nini matokeo ya kuchukia huku kwa kupindukia? Ni kwamba Mungu atamweka pembeni mtu huyu, na kutomwitikia kwa sasa. Kisha atasubiri sasa kuwashughulikia “baada ya msimu wa kupukutika kwa majani.” Hali hii inaashiria nini? Mtu huyu angali anayo matokeo? Mungu hakuwahi kunuia kumpa mtu wa aina hii matokeo! Hivyo basi si jambo la kawaida endapo Mungu kwa sasa hamwitikii mtu wa aina hii? (Ndiyo.) Mtu wa aina hii anafaa kujitayarisha vipi sasa? Wanafaa kujitayarisha kukabiliana na zile athari mbaya zilizosababishwa na tabia zao na maovu waliofanya. Huu ndio mwitikio wa Mungu kwa mtu wa aina hii. Hivyo basi Nasema waziwazi kwa mtu wa aina hii: Usishikilie imani za uwongo tena, na usijihusishe katika kufikiria makuu tena. Mungu hatavumilia watu siku zote bila kikomo; Hatastahimili dhambi zao au kutotii kwao bila kukoma. Baadhi ya watu watasema: “Nimeweza pia kuona watu wachache kama hawa. Wanapoomba wanaguswa hasa na Mungu, na wanalia

kwa machungu. Kwa kawaida wao pia wanakuwa na furaha sana; wanaonekana kuwa na uwepo wa Mungu, na mwongozo wa Mungu.” Usiseme huo upuzi! Kulia kwa machungu si lazima iwe kwamba umeguswa na Mungu au unao uwepo wa Mungu, acha hata mwongozo wa Mungu. Kama watu watamghadhabisha Mungu, je, bado Mungu atawaongoza? Nikiongea kwa ujumla, wakati Mungu ameamua kumwondoa mtu, kuwaacha watu hao, tayari mtu huyo hana matokeo. Haijalishi ni vipi wanavyohisi kutosheka kujihusu wao wenyewe wakati wanapoomba, na imani kiwango kipi walichonacho katika Mungu mioyoni mwao; tayari hii si muhimu. Kitu cha muhimu ni kwamba Mungu hahitaji aina hii ya imani kwamba Mungu tayari amemsukumia mbali mtu huyu. Namna ya kuwashughulikia baadaye pia si muhimu. Kilicho muhimu ni kwamba katika muda ule ambao mtu huyu atamghadhabisha Mungu, matokeo yao tayari yameanzishwa. Kama Mungu ameamua kutomwokoza mtu wa aina hii, basi ataachwa na kuadhibiwa. Huu ndio mwelekeo wa Mungu.

Ingawa sehemu ya kiini halisi cha Mungu ni upendo, na Anaitoa rehema yake kwa kila mtu, watu hupuuza na kusahau hoja kwamba kiini Chake halisi ni heshima vilevile. Kwamba Anao upendo haimaanishi kwamba watu wanaweza kumkosea Yeye wapendavyo na kwamba Yeye hana hisia zozote, au mijibizo yoyote. Kwamba Anayo rehema haimaanishi kwamba Hana kanuni zozote kuhusiana na namna Anavyoshughulikia watu. Mungu yu hai; kwa kweli Yupo. Yeye si kikaragosi kilichofikiriwa au kitu kingine tu. Kwa sababu Yeye yupo, tunafaa kusikiliza kwa makini sauti ya moyo Wake siku zote, kutilia makini mwelekeo Wake, na kuzielewa hisia Zake. Hatufai kutumia kufikiria kwa watu ili kumfafanua Mungu, na hatufai kulazimisha fikira na matamania ya watu kwa Mungu, kumfanya Mungu kutumia mtindo na fikira za binadamu katika namna Anavyomshughulikia binadamu. Ukifanya hivyo, basi unamghadhabisha Mungu, unaijaribu hasira ya Mungu, na unapinga heshima ya Mungu! Hivyo basi, baada ya kuelewa ukali na uzito wa suala hili, Ninasihi kila mmoja wenu mlio hapa kuwa makini na wenye busara katika vitendo vyenu. Kuwa makini na wenye busara katika kuongea kwenu. Na kuhusiana na namna mnavyoshughulikia Mungu, mnapokuwa makini zaidi na wenye busara zaidi, ndivyo ilivyo bora zaidi! Wakati huelewi mwelekeo wa Mungu ni nini, usizungumze kwa uzembe, usiwe mzembe katika vitendo vyako, na usipachike majina ovyo ovyo. Na hata zaidi, usikimbilie hitimisho kiholela. Badala yake, unafaa kusubiri na kutafuta; hili pia ndilo dhihirisho la kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Kama unaweza kutimiza hoja hii kati ya zote, na kumiliki mwelekeo huu kati ya yote, basi Mungu hatakulaumu wewe kwa upumbavu wako, kutojua kwako, na ukosefu wa kuelewa kwa sababu zinazosababisha vitu. Badala yake, kutokana na hofu yako ya kumkosea Mungu, heshima yako kwa nia za Mungu, na mwelekeo wako wa kuwa radhi kumtii Yeye, Mungu atakukumbuka, atakuongoza na kukuangaza wewe, au kustahimili kutokuwa mkomavu kwako na kutojua kwako. Kinyume chake, endapo mwelekeo wako kwake

Yeye utakuwa usioheshimu—kuhukumu Mungu kiholela, kukisia kiholela, na kufafanua maana ya Mungu—Mungu atakupa hukumu, nidhamu, au hata adhabu; au Atakupa taarifa. Pengine kauli hii inahusisha matokeo yako. Hivyo basi, Ningali bado nataka kutilia mkazo jambo hili kwa mara nyingine: Unapaswa uwe makini na mwenye busara katika kila kitu kinachotoka kwa Mungu. Usiongee kwa uzembe, na usiwe mzembe katika matendo yako. Kabla ya kusema chochote, unafaa kufikiria: Je, kufanya hivi kutamghadhabisha Mungu? Kufanya hivi ni kumcha Mungu? Hata katika masuala mepesi, bado unafaa kujaribu kuelewa hakika maswali haya, yafikirie kwa kweli. Kama unaweza kwa kweli kutenda haya kulingana na kanuni hizi kila pahali, katika hali zote, katika vitu vyoye, nyakati zote, na kushikilia mtazamo wa aina hiyo hasa wakati huelewi kitu basi Mungu siku zote atakuongoza wewe, na kukupa na hata njia ya kufuata. Bila kujali ni nini ambacho watu wanaonyesha, Mungu anaona yote waziwazi, dhahiri, na Atakupa utathmini sahihi na unaofaa kwa maonyesho haya. Baada ya kupitia jaribio la mwisho, Mungu atachukua tabia yako yote na kuijumlisha ili kuasisi matokeo yako. Matokeo haya yatashawishi kila mmoja bila shaka lolote. Kile ambacho Ningependa kuwaambia ni kwamba kila kitendo chenu, kila hatua yenu, na kila fikira yenu vyote vitaamua majaliwa yenu.

Ni Nani Hupanga Matokeo ya Binadamu

Kunalo jambo jingine muhimu zaidi, na hilo ni mwelekeo wenu kwa Mungu. Mwelekeo huu ni muhimu sana! Huamua kama hatimaye mtatembea kuelekea katika maangamizo, au kwenye hatima nzuri na ya kupendeza ambayo Mungu amewatayarishia. Katika Enzi ya Ufalme, Mungu tayari amefanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 na kwenye kipindi cha miaka hii 20 pengine mioyo yenu imekuwa na tashwishi kuhusu utendakazi wenu. Hata hivyo, katika moyo wa Mungu, Ameweka rekodi halisi na ya kweli kwa kila mmoja wenu. Kuanzia wakati ule ambao kila mtu anaanza kumfuata Yeye na kusikiliza mahubiri Yake, kuelewa zaidi na zaidi kuhusu ukweli, hadi pale ambapo wanatekeleza wajibu wao—Mungu anayo rekodi ya kila mojawapo ya maonyesho haya. Wakati mtu anapofanya wajibu wake, wakati anapokabiliwa na kila aina ya hali, kila aina ya majaribio, mwelekeo wa mtu huyo ni upi? Wanatenda kazi vipi? Wanahisi vipi kwa Mungu katika mioyo yao? ... Mungu ameweka rekodi ya yote haya, rekodi yote kwa hakika. Pengine kutokana na mtazamo wenu, masuala haya yanakanganya. Hata hivyo, kutoka pale ambapo Mungu yupo, yote yako wazi kabisa, na hakuna hata dalili yoyote ya kutokuwa wazi. Hili ni suala linalohusisha matokeo ya kila mmoja, na majaliwa yao na matarajio yao ya siku za baadaye vilevile. Hata zaidi, hapa ndipo ambapo Mungu anatumia jitihada Zake zote alizomakinikia. Hivyo basi Mungu hathubutu kuipuuza hata kidogo, na hatavumilia kutomakinika kokote. Mungu anarekodi haya yote kuhusu wanadamu, anarekodi mambo kuhusu mkondo mzima wa binadamu anayefuata Mungu, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mwelekeo wako kwa Mungu wakati huu utaamua hatima yako. Je, haya si kweli? Kutoka hapo mpaka sasa,

mnasadiki kwamba Mungu ni mwenye haki? Vitendo vya Mungu vinafaa? Bado mnayo picha yoyote ya Mungu vichwani mwenu? (La.) Basi mnasema kwamba matokeo ya binadamu ni kwa ajili ya Mungu kuweza kupanga au kwa ajili ya binadamu mwenyewe kupanga? (Ni kwa Mungu kupanga.) Ni nani basi anayeyapanga? (Mungu.) Hamna hakika, sivyo? Ndugu kutoka makanisa ya Hong Kong, ongeeni—ni nani anayeyapanga? (Binadamu anayapanga mwenyewe.) Mwanadamu anayapanga? Hivyo basi haimaanishi kwamba haina chochote kuhusu Mungu? Ndugu kutoka Korea Kusini, ongeeni. (Mungu huanzisha matokeo ya binadamu kutokana na hatua na vitendo vyake vyote na kutokana pia na njia wanayotembelea.) Hili ni jibu halisi sana. Kunayo hoja hapa ambayo lazima Niwafahamishe nyinyi: Kwenye mkondo wa kazi ya wokovu wa Mungu, Yeye huweka kiwango kwa binadamu. Kiwango hiki ni kwamba binadamu anaweza kutii neno la Mungu, na kutembea kwa njia ya Mungu. Ndicho kiwango kinachotumika kupima matokeo ya binadamu. Kama utafanya mazoezi kwa mujibu wa kiwango hiki cha Mungu, basi unaweza kupata matokeo mazuri; kama hutafanya hivyo, basi huwezi kupokea matokeo mazuri. Basi ni nani unayesema kwamba anayapanga matokeo haya? Si Mungu pekee anayeyapanga, lakini badala yake Mungu na binadamu pamoja. Hiyo ni sahihi? (Ndiyo.) Kwa nini hivyo? Kwa sababu ni Mungu ambaye anataka kujishughulisha na kujihusisha katika kazi ya wokovu wa wanadamu, na kutayarisha hatima nzuri kwa ajili ya binadamu; binadamu ndiye mlengwa wa kazi ya Mungu, na matokeo haya, hatima hii, ndiyo ambayo Mungu humtayarishia binadamu. Kama kusingekuwa na kilengwa cha kazi Yake, basi Mungu asingehitaji kazi hii; kama Mungu asingefanya kazi hii, basi binadamu asingekuwa na fursa ya wokovu. Binadamu ndiye mlengwa wa wokovu, na ingawa binadamu yumo kwenye upande wa kimya katika mchakato huu, ni mwelekeo wa upande huu ambao unaamua kama Mungu atafanikiwa katika kazi Yake ya kuwaokoa wanadamu au la. Kama si mwongozo ambao Mungu anakupa wewe, basi usingejua kiwango Chake, na usingekuwa na lengo lolote. Kama unacho kiwango hiki, lengo hili, ilhali hushirikiani, hilitili kwenye matendo, hulipii gharama, basi bado hutapokea matokeo haya. Kwa sababu hii, Ninasema kwamba matokeo haya hayawezi kutenganishwa na Mungu, na pia hayawezi kutenganishwa na binadamu. Na sasa unaweza kujua ni nani anayepanga matokeo ya binadamu.

Watu Huishia Kumfafanua Mungu Kutokana na Uzoefu Wao

Wakati wa kuwasilisha mada ya kumjua Mungu, mmegundua kitu? Mmegundua kwamba mwelekeo wa sasa wa Mungu umepitia mabadiliko? Je, mwelekeo wa Mungu kwa wanadamu hauwezi kubadilika? Je, siku zote Mungu atavumilia hivi, huku akimpa upendo Wake wote na rehema kwa binadamu bila kikomo? Suala hili pia linahusu kiini halisi cha Mungu. Hebu turejeele swali la yule mtoto wa kiume mbadhirifu kama aitwavyo kutoka awali. Baada ya swali hili kuulizwa, majibu yenu hayakuwa wazi sana. Kwa maneno mengine, bado hamwelewi vizuri

nia za Mungu. Punde tu watu wanapojua kwamba Mungu anawapenda wanadamu, wanamfafanua Mungu kama ishara ya upendo: Haijalishi kile wanachofanya watu, haijalishi namna wanavyotenda mambo, haijalishi vipi wanavyomshughulikia Mungu na haijalishi ni vipi wasivyotii, hakuna chochote kinachojalisha kwa sababu Mungu ni upendo na upendo wa Mungu hauna mipaka na haupimiki. Mungu anao upendo, hivyo basi Anaweza kuvumilia watu; Mungu anao upendo, hivyo basi Anaweza kuwa mwenye rehema kwa watu, mwenye rehema kwa kutokomaa kwao, mwenye rehema kwa kutojua kwao, na mwenye rehema kwa kutotii kwao. Hivi ndivyo ilivyo kwa kweli? Kwa baadhi ya watu, wakati wamepitia subira ya Mungu mara moja, au mara chache, watashughulikia suala hili kama mtaji katika uelewa wao wa Mungu, wakisadiki kwamba Mungu atakuwa mara moja na milele mwenye subira kwao, atakuwa mwenye rehema kwao, na kwenye mkondo wa maisha yao watachukua subira ya Mungu na kuichukulia kama kiwango cha ni vipi ambavyo Mungu anawashughulikia. Kunao pia watu ambao, wakati wamepitia uvumilivu wa Mungu mara moja, daima watamfafanua Mungu kuwa uvumilivu, na uvumilivu huu hauna mipaka, hauna masharti, na hata usio na kanuni zozote. Je, kusadiki huku ni sahihi? Kila wakati mambo kuhusu kiini cha Mungu au tabia ya Mungu yanapozungumziwa, mwaonekana mmechanganywa mno. Kuwaona mkiwa hivi kunanifanya Mimi kuwa na wasiwasi. Mmeusikia mambo mengi ya ukweli kuhusiana na kiini halisi cha Mungu; mmeweza pia kusikiliza mada mengi kuhusiana na tabia ya Mungu. Hata hivyo, katika akili zenu masuala haya, na ukweli wa dhana hizi, ni kumbukumbu tu kutokana na nadharia na maneno yaliyoandikwa. Hakuna kati yenu anaweza kupitia kile ambacho tabia ya Mungu inamaanisha katika maisha yenu halisi, wala hamwezi kuona tu tabia ya Mungu ni nini. Hivyo basi, nyote mmechanganyikiwa katika kusadiki kwenu, nyote mnasadiki bila kujua, hadi kufikia kiwango ambacho mnao mwelekeo usiofaa kwa Mungu, kwamba mnamweka pembeni. Mwelekeo kama huu kwa Mungu unawaongoza wapi? Mnaongozwa katika hali ya kutoa hitimisho siku zote kuhusu Mungu. Punde unapopata maarifa kidogo, unahisi umetosheka kweli, unahisi ni kana kwamba umempokea Mungu kwa uzima Wake wote. Baadaye unahitimisha kwamba hivi ndivyo Mungu Alivyo, na humruhusu kuendelea mbele na shughuli Zake kwa furaha zaidi. Na kila Mungu anapofanya jambo jipya, hukubali kwamba Yeye ni Mungu. Siku moja, wakati Mungu atakaposema: “Simpendi binadamu tena; Sitoi rehema kwa binadamu tena; Sina uvumilivu au subira yoyote kwa binadamu tena; Nimejaa chuki na uhasama kupindukia kwa binadamu,” watu watakinzana na aina hii ya taarifa kutoka kwenye ndani ya mioyo yao. Baadhi yao wataweza hata kusema: “Wewe si Mungu wangu tena; Wewe si Mungu ninayetaka kufuata tena. Kama hivi ndivyo Unavyosema, basi Hujafuzu tena kuwa Mungu wangu, na sitaki kuendelea kukufuata Wewe. Kama Hunipi rehema, hunipi upendo, hunipi uvumilivu, basi nami sitakufuata Wewe tena. Kama Utakuwa mvumilivu tu kwangu bila kikomo, utakuwa mwenye subira kwangu mimi, na kuniruhusu mimi kuona kwamba Wewe ni upendo, kwamba Wewe ni

subira, kwamba Wewe ni uvumilivu, hapo tu ndipo nitakapoweza kukufuata Wewe, na hapo tu ndipo nitakapoweza kuwa na ujasiri kukufuata mpaka mwisho. Kwa sababu ninapata subira na rehema Yako, kutotii kwangu na dhambi zangu zinaweza kusamehewa bila kikomo, kuondolewa bila kikomo, na ninaweza kutenda dhambi wakati wowote na mahali popote, kutubu na kusamehewa wakati wowote na mahali popote, na kukughadhabisha wakati wowote na mahali popote. Hufai kuwa na fikira au hitimisho Zako binafsi kuhusiana na mimi.” Ingawa huenda usifikirie kuhusu aina hii ya swali kwa namna ya kibinafsi na ya kufahamu kama hiyo, kila unapomchukulia Mungu kuwa zana ya dhambi zako kusamehewa na kifaa cha kutumika cha kupata hatima nzuri, tayari unamweka kwa njia isiyoeleweka Mungu aliye hai na katika hali ya kukupinga wewe, kuwa adui yako. Hivi ndivyo Ninavyoona. Unaweza kuendelea kusema, “Ninasadiki Mungu”; “Ninafuatilia ukweli”; “Ninataka kubadilisha tabia yangu”; “Ninataka kuwa huru dhidi ya ushawishi wa giza”; “Ninataka kumtosheleza Mungu”; “Nataka kumtii Mungu”; “Ninataka kuwa mwaminifu kwa Mungu, na kufanya wajibu wangu vizuri”; na kadhalika. Hata hivyo; haijalishi ni vipi utakavyosema kinasikika kuwa kizuri, haijalishi ni nadharia kiasi kipi unayojua, haijalishi ni vipi nadharia hiyo inavyovutia, ni vipi nadharia hiyo ilivyo na heshima, hoja ya mambo ni kwamba kunao wengi wenu ambao tayari wamejifunza namna ya kutumia taratibu, falsafa, nadharia mlizojifunza katika kuhitimisha mambo kuhusu Mungu, na kumweka yeye katika upinzani na nyinyi wenyewe kwa njia ambayo ni ya kimaumbile kabisa. Ingawa umejifunza barua na kujifunza falsafa, bado hujaingia kwa hakika katika uhalisia wa ukweli, hivyo basi ni vigumu sana kwako kuwa karibu na Mungu, kumjua Mungu, na kumwelewa Mungu. Hali hii inasikitisha!

Niliiona picha hii kwenye video: Akina dada wachache walikuwa wameshikilia kitabu cha Neno Laonekana katika Mwili, na walikuwa wamekishikilia juu sana. Walikuwa wamekishikilia kitabu hiki kikiwa katikati yao, na juu zaidi kuliko vichwa vyao. Ingawa hii ni picha tu, kile kilichoamshwa ndani Yangu si picha. Badala yake, hiyo picha ilinifanya kufikiria kwamba kile ambacho kila mtu hushikilia juu angani kwenye mioyo yao si neno la Mungu, lakini ni kitabu cha neno la Mungu. Hili ni suala la kusikitisha moyo sana. Njia hii ya kutenda mambo si njia kwa kweli ya kumshikilia Mungu kwa heshima. Ni kwa sababu hamwelewi Mungu kiasi cha kwamba swali wazi, swali dogo sana, linawafanya kuja na mawazo yenu binafsi. Wakati Ninapowauliza maswali, wakati Ninapomakinika na ninyi, mnajibu kwa kubahatisha na kwa kutumia kufikiria kwenu binafsi; baadhi yenu hata huchukua sauti ya shaka na kuuliza tena swali hilo kwangu. Hii inathibitisha hata waziwazi kwangu Mimi kwamba yule Mungu mnayemsadiki si Mungu wa kweli. Baada ya kulisoma neno la Mungu kwa miaka mingi sana, mnalitumia neno la Mungu, kutumia kazi ya Mungu, na falsafa nyingi zaidi katika kuhitimisha mengi kuhusu Mungu kwa mara nyingine. Aidha, hamjawahi kujaribu kumwelewa Mungu; hamjawahi kujaribu

kupata kuelewa nia za Mungu; hufanyi jaribio la kuelewa mwelekeo wa Mungu kwa binadamu ni nini; au ni vipi ambavyo Mungu anafikiria, kwa nini Anayo huzuni, kwa nini Anayo ghadhabu, kwa nini Yeye husukumia watu mbali, na maswali mengine kama hayo. Na kwa kuongezea hayo, watu wengi zaidi wanasadiki kwamba Mungu siku zote amekuwa kimya kwa sababu Anaangalia tu vitendo vya wanadamu, kwa sababu Hana mwelekeo wowote kwao, wala Hana fikira zozote Zake binafsi. Kundi jingine linasukumiza mbele zaidi suala hili. Watu hawa wanaamini kwamba Mungu hatamki neno kwa sababu Amekubali, Mungu hatamki neno kwa sababu Anasubiria, Mungu hatamki neno kwa sababu Hana mwelekeo, kwa sababu mwelekeo wa Mungu tayari umefafanuliwa kwa kina ndani ya vitabu, tayari umeelezewa kwa uzima wake kwa wanadamu, na hauhitajiki kurudiwa kwa watu mara kwa mara. Ingawa Mungu yuko kimya, bado Anao mwelekeo, anao mtazamo, na anacho kiwango ambacho Anahitaji kutoka kwa watu. Ingawa watu hawajaribu kumwelewa Yeye, na hawajaribu kumtafuta Yeye, mwelekeo Wake uko wazi sana. Fikiria mtu ambaye aliwahi kumfuata Mungu kwa shauku, lakini wakati fulani akaacha kumfuata Yeye na akaondoka. Mtu huyu akitaka kurudi sasa, jambo la kushangaza ni kwamba, hamjui mtazamo wa Mungu utakuwa upi, na mwelekeo wa Mungu utakuwa upi. Hili si jambo ovyo? Kwa hakika, hili ni suala ambalo kwa kiasi fulani ni la juujuu. Kama kweli mngeelewa moyo wa Mungu, mngejua mwelekeo Wake kwa mtu wa aina hii, na msingelitoa jibu la juujuu. Kwa sababu hamjui, Niruhusu kuwafafanulia pale msipoelewa.

Mwelekeo wa Mungu kwa Wale Wanaotoroka Wakati Kazi Yake Inaendelea

Utampata mtu wa aina hii kila pahali: Baada ya kuwa na hakika kuhusu njia ya Mungu, kwa sababu mbalimbali, wanaondoka kimyakimya bila ya neno la kwaheri na kufanya chochote kile ambacho moyo wao unatamani. Huku haya yakiendelea, hatutaingilia kwa nini mtu huyu anaondoka. Kwanza tutaangalia mwelekeo wa Mungu ni upi kwa mtu wa aina hii. Iko wazi sana! Tangu muda ule ambao mtu huyu huondoka, machoni mwa Mungu, kile kipindi cha imani yao kimekwisha. Si mtu huyu aliyekimaliza, bali ni Mungu. Kwamba mtu huyu alimwacha Mungu inamaanisha kwamba tayari amemkataa Mungu, kwamba tayari hamtaki Mungu. Inamaanisha kwamba tayari hakubali wokovu wa Mungu. Kwa sababu mtu huyu hamtaki Mungu, Mungu naye anaweza bado kumtaka? Aidha wakati mtu huyu anao mwelekeo huu, mtazamo huu, na anayo azma ya kumwacha Mungu, tayari ameikera tabia ya Mungu. Hata ingawa hawakujipata wakiwa na hasira na wakalaani Mungu, hata ingawa hawakujihusisha katika uovu wowote au tabia au utovu wa nidhamu, na hata ingawa mtu huyu hafikirii: Kama kutawahi kuwepo na siku nitakapokuwa nimeshiba anasa zangu kwa nje, au nitakapokuwa bado nahitaji kitu kutoka kwa Mungu, nitarudi. Au kama Mungu ataniita, nitarudi. Au wanasema: Kama nitajeruhiwa kwa nje, nikiuona ulimwengu wa nje una giza sana na una maovu sana na sitaki tena kujishirikisha nao, nitarudi kwa Mungu. Hata ingawa mtu huyu amepiga hesabu katika akili zake ni wakati gani

anarudi, hata ingawa wanauacha mlango ukiwa wazi wa kurudi kwao, hawatambui kwamba bila kujali ni namna gani wanavyofikiria na namna gani wanavyopanga, hii ni ndoto tu. Kosa lao kubwa zaidi ni kutokuwa wazi kuhusu namna ambavyo Mungu anahisi wakati wanapotaka kuondoka. Kuanzia muda ule ambao mtu huyu anaamua kumwacha Mungu, Mungu amemwacha kabisa; tayari Mungu ameanzisha matokeo katika moyo Wake. Matokeo hayo ni yapi? Kwamba mtu huyu ni mmoja wa buku, na ataangamia pamoja nao. Hivyo basi, watu mara nyingi huona aina hii ya hali: Mtu anamwacha Mungu, lakini hapokei adhabu yoyote. Mungu hufanya kazi kulingana na kanuni Zake binafsi. Watu wanaweza kuona baadhi ya mambo, na baadhi ya mambo yanahitimishwa tu katika moyo wa Mungu, kwa hivyo watu hawawezi kuyaona matokeo. Kile ambacho watu huona si lazima kiwe ndio upande wa ukweli wa mambo; lakini upande ule mwingine, ule upande usiouona—hizi ndizo fikira na hitimisho la kweli kuhusu moyo wa Mungu.

Watu Wanaotoroka Wakati wa Kazi ya Mungu ni Wale Wanaoiacha Njia ya Kweli

Hivyo basi kwa nini Mungu ampe mtu wa aina hii adhabu kali kama hiyo? Kwa nini Mungu anakuwa na hasira kali kwao? Kwanza kabisa tunajua kwamba tabia ya Mungu ni adhama, ni hasira. Yeye si kondoo ili achinjwe na yeyote; na hata zaidi Yeye si kikaragosi ili adhibitiwe na watu vyovyote vile wanavyotaka. Yeye pia si hewa tupu ili kuamrisha huku na kule na watu. Kama kweli unasadiki kwamba Mungu yupo, unafaa kuwa na moyo unaomcha Mungu, na unafaa kujua kwamba kiini halisi cha Mungu hakifai kughadhabishwa. Ghadhabu hii inaweza kusababishwa na neno; pengine fikira; pengine aina fulani ya tabia bovu; pengine tabia ya upole tabia inayoweza kuruhusiwa kwenye macho na maadili ya binadamu; au pengine inasababishwa na falsafa, nadharia. Hata hivyo, punde unapomghadhabisha Mungu, fursa yako inapotea na siku zako za mwisho zinakuwa zimewasili. Hili ni jambo baya! Kama huelewi kwamba Mungu hawezi kukosewa, basi pengine humchi Mungu, na pengine unamkosea Yeye kila wakati. Kama hujui namna ya kumcha Mungu, basi huwezi kumcha Mungu, na hutaweza kujua namna ya kujiweka kwenye njia ya kutembelea kwa njia ya Mungu—kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Punde unapokuwa na habari, unaweza kuwa na ufahamu kwamba Mungu hawezi kukosewa, kisha utajua ni nini maana ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu.

Kutembea katika njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu si lazima kuumaanisha ni kiwango kipi cha ukweli unachojua, ni majaribio mangapi ambayo umepitia, au ni mitihani mingapi ambayo umepitia na kutiwa adabu. Badala yake, kunategemea aina ya mtazamo ulio nao kwa Mungu moyoni mwako, na kiini unachokionyesha. Kiini halisi cha watu na mielekeo yao ya kibinafsi—mambo haya ni muhimu sana, muhimu kabisa. Kuhusiana na wale watu ambao wamemkana na kumwacha Mungu, mwelekeo wao wa dharau kwa Mungu na mioyo yao

inayodharau ukweli ulikera tabia ya Mungu, hivyo basi kulingana na Mungu hawatawahi kusamehewa. Wamejua kuhusu uwepo wa Mungu, wamekuwa na taarifa kwamba Mungu tayari amewasili, wameweza hata kupitia kazi mpya ya Mungu. Kuondoka kwao si kutokana na kudanganywa, wala si suala kwamba wao wamechanganyikiwa kulihusu. Hata si suala hata kidogo la wao kulazimishwa kuondoka. Lakini kwa nadhari yao, na kwa akili iliyo wazi, wamechagua kumwacha Mungu. Kuondoka kwao si kupotea kwao; si hata kutupwa kwao nje. Hivyo basi, katika macho ya Mungu, wao si kondoo aliyepotea njia kutoka kwenye kondoo wale wengine, sikuambii hata mtoto wa kiume mbadhirifu aliyepotea njia yake. Waliondoka bila hofu ya kuadhibiwa, na hali kama hiyo, mfano kama huo unaikera tabia ya Mungu na ni kutokana na kero hili ambapo Yeye huwapa matokeo yasiyo na matumaini. Je, huoni kwamba matokeo kama haya yanatisha? Hivyo basi kama watu hawamjui Mungu, wanaweza kumkosea Mungu. Hilo ni suala dogo! Kama mtu hatachukulia mwelekeo wa Mungu kwa umakinifu, na bado anasadiki kwamba Mungu angali anatarajia kurudi kwake—kwa sababu wao ni mojawapo wa kondoo wa Mungu waliopotea na kwamba Mungu angali anawasubiria kubadilisha moyo wao—basi mtu huyu hayupo mbali sana na kuweza kuondolewa kwenye siku yake ya adhabu. Mungu hatakataa tu kumkaribisha. Hii ndiyo mara yake ya pili ya kuikera tabia ya Mungu; hivyo basi suala hili ni baya zaidi! Mwelekeo wa mtu huyu usioheshimu vitu vitakatifu tayari umekosea agizo la kiutawala la Mungu. Bado Mungu atawakaribisha? Kwa moyo Wake, kanuni za Mungu kuhusiana na suala hili ni kwamba mtu amefikia uhakika kuhusu ni ipi ndiyo njia ya kweli, ilhali anaweza bado kwa nadhari yake na kwa akili wazi kumkataa Mungu, na kuondoka kutoka kwa Mungu, basi Mungu atazuia kabisa barabara iendayo katika wokovu wake, na hata lango la kuingia kwenye ufalme watafungiwa. Wakati mtu huyu atakapokuja kubisha kwa mara nyingine, Mungu hatamfungulia lango. Mtu huyu atafungiwa milele. Pengine baadhi yenu mmeisoma hadithi hii ya Musa kwenye Biblia. Baada ya Musa kupakwa mafuta na Mungu, viongozi 250 walionyesha ukosefu wa utiifu kwa Musa kwa sababu ya hatua zake na sababu nyinginezo mbalimbali. Ni nani waliyekataa kumtii? Hakuwa Musa. Walikataa kutii mipango ya Mungu; walikataa kutii kazi ya Mungu katika suala hili. Walisema yafuatayo: “Ninyi mnachukua mengi kwenu, kwa sababu mkusanyiko wote ni mtakatifu, kila mmoja wao, naye Yehova yuko miongoni mwao....” Katika macho yenu, maneno haya ni mazito? Si mazito! Angaa maana ya moja kwa moja ya maneno haya si mazito. Katika mkondo wa kisheria, hawavunji sheria zozote, kwa sababu kwenye sehemu ya juu kabisa si lugha katili, au msamiati, isitoshe, hayana maana yoyote ya kukufuru. Sentensi ya kawaida ndiyo iliyo hapo, hamna cha ziada. Ilhali inakuwaje kwamba maneno haya yanaweza kuanzisha hasira kali kama hiyo kutoka kwa Mungu? Ni kwa sababu hayasemwi kwa watu, mbali kwa Mungu. Mwelekeo na tabia iliyoelezewa na wao ndicho hasa kinachoikera tabia ya Mungu, na wao wanaikosea tabia ya Mungu ambayo haipaswi kukosewa. Sote tunajua matokeo yao hatimaye yalikuwa yapi. Kuhusiana na wale waliomwacha

Mungu, mtazamo wao ni upi? Mwelekeo wao ni upi? Na ni kwa nini mtazamo na mwelekeo wao unasababisha Mungu kuwashughulikia kwa njia hiyo? Sababu ni kwamba wanajua waziwazi Yeye ni Mungu ilhali bado wanachagua kumsaliti Yeye. Na ndiyo maana wanaondolewa kabisa fursa yao ya wokovu. Kama vile Biblia inavyosema: “Kwa sababu tukitenda dhambi makusudi baada ya sisi kupokea maarifa ya ukweli, hakuna tena dhabihu ya dhambi.” Je, mmelielewa suala hili sasa?

Majaliwa ya Binadamu Yanaamuliwa na Mwelekeo Wake Kwa Mungu

Mungu ni Mungu aliye hai, na kama vile tu watu wanavyotenda tofauti katika hali tofauti, ndivyo mwelekeo wa Mungu ulivyo katika utendakazi huu na unavyotofautiana kwa sababu Yeye si kikaragosi, wala Yeye si hewa tupu. Kupata kuujua mwelekeo wa Mungu ni jambo lenye thamani kwa wanadamu. Watu wanafaa kujifunza vipi, kwa kuujua mwelekeo wa Mungu, wanaweza kuijua tabia ya Mungu na kuuelewa moyo Wake kidogo kidogo. Unapouelewa moyo wa Mungu kidogo kidogo hutahisi kwamba kumcha Mungu na kujiepusha na maovu ni jambo gumu la kutimiza. Kilicho zaidi ni kwamba, unapomwelewa Mungu, hakuna uwezekano wa wewe kufanya hitimisho kuhusu Yeye. Unapoacha kufanya hitimisho kuhusu Mungu, hakuna uwezekano wa wewe kumkosea Yeye, na bila kujua Mungu atakuongoza kuwa na maarifa Yake, na hivyo basi utamcha Mungu katika moyo wako. Utaacha kumfafanua Mungu kwa kutumia falsafa, zile barua, na nadharia ambazo umejifunza. Badala yake, kwa kutafuta nia za Mungu katika mambo yote na siku zote utaweza bila kufahamu kuwa mtu anayefuata moyo wa Mungu.

Kazi ya Mungu haionekani wala kugusika na wanadamu, lakini kulingana na Mungu, hatua za kila mmoja, pamoja na mwelekeo wake kwake Yeye—haya hayatambuliki tu na Mungu, lakini pia kuonekana vilevile. Hili ni jambo ambalo kila mmoja anafaa kutambua na kuwa wazi kuhusu. Unaweza kuwa ukijiuliza siku zote: “Je, Mungu anajua kile ninachofanya hapa? Je, Mungu anajua kile ninachofikiria sasa hivi? Pengine Anajua, pengine Hajui.” Kama utakuwa na aina hii ya mtazamo, kufuata na kusadiki Mungu ilhali unatia shaka katika kazi Yake na uwepo Wake, basi hivi karibuni au baadaye siku itawadia ambapo utamghadhabisha, kwa sababu tayari unayumbayumba pembezoni pa jabali hatari. Nimewaona watu ambao wamesadiki katika Mungu kwa miaka mingi lakini bado hawajapata uhalisia wa ukweli, wala hawaelewi hata mapenzi ya Mungu. Maisha yao na kimo chao havipigi hatua yoyote, ukitii tu falsafa zile za kiwango cha chini zaidi. Hii ni kwa sababu watu hawa hawajawahi kuchukulia neno la Mungu kama maisha yao binafsi, na hawajawahi kukabiliana na kukubali uwepo Wake. Je, unafikiri kwamba Mungu huwaona watu kama hawa na kujawa na furaha? Je, wanamtuliza Yeye? Katika jinsi hiyo, ni mbinu ya imani ya watu katika Mungu ambayo inaamua majaliwa yao. Kuhusu jinsi watu humtafuta na jinsi wanavyomweleka Mungu, mitazamo ya watu ni ya umuhimu wa

kimsingi. Usimwache Mungu kana kwamba yeye ni fungu la hewa kavu tu linaloelea karibu na nyuma ya kichwa chako. Usikose kumjali Mungu ni kana kwamba Yeye ni hewa tupu nyuma ya kichwa chako. Siku zote fikiria kuhusu Mungu wa imani yako kama Mungu hai, Mungu halisi. Yeye hayupo kule juu kwenye mbingu ya tatu bila chochote cha kufanya. Badala yake, siku zote bila kusita Anaangalia kwenye mioyo ya kila mmoja, Akiangalia ni nini unachofanya, akichunguza kila neno dogo na kila tukio dogo, akiangalia mwenendo wako na mwelekeo wako kwa Mungu. Kama uko radhi kujitolea kwa Mungu au la, tabia yako yote na fikira zako na mawazo yako ya ndani zaidi ziko mbele ya Mungu, na yanaangaliwa na Yeye. Ni kulingana na tabia yako, kulingana na vitendo vyako, na kulingana na mwelekeo wako kwa Mungu, ambapo maoni Yake kwako, na mwenendo Wake kwako, vinaendelea vikibadilika. Mimi Ningependa kutoa ushauri fulani kwa baadhi ya watu. Msijiweke kwenye mikono ya Mungu kama watoto wachanga, kana kwamba Yeye Anapaswa kukupenda sana, kana kwamba Asingewahi kukuacha, na kana kwamba mwelekeo Wake kwako ni imara na usingeweza kubadilika, na Ninawashauri muache kuota ndoto! Mungu ni mwenye haki katika kutendea kila mtu. Anakabiliana na kazi ya ushindi wa wanadamu na wokovu kwa bidii. Huo ndio usimamizi Wake. Anashughulikia kila mmoja kwa umakinifu, na wala si kama kiumbe cha kufugwa cha kucheza nacho. Upendo wa Mungu kwa binadamu si ule wa kudekeza au kupotosha; rehema na uvumilivu Wake kwa wanadamu si dokezi au ya kutotilia maanani. Kinyume cha mambo, upendo wa Mungu kwa wanadamu ni wa kutunza, kusikitikia, na kuheshimu maisha; rehema na uvumilivu Wake vyote vinaonyesha matarajio Yake kwa binadamu; rehema na uvumilivu Wake ndivyo ambavyo binadamu anahitaji ili kuishi. Mungu yuko hai, na kwa hakika Mungu yupo; mwelekeo Wake kwa wanadamu unafuata kanuni, si yenye kutangazwa kama imani ya dini, na unaweza kubadilika. Mapenzi Yake kwa binadamu yanabadilika kwa utaratibu na kurekebishwa kwa muda, hali na mwelekeo wa kila mtu. Kwa hiyo, unafaa kujua rohoni mwako na uwazi wote kwamba kiini halisi cha Mungu hakibadiliki, na kwamba tabia Yake itajitokeza katika nyakati tofauti, na muktadha tofauti. Huenda usifikirie kwamba hili si suala muhimu, na wewe unatumia dhana zako za kibinafsi katika kufikiria namna ambavyo Mungu anafaa kufanya mambo. Lakini zipo nyakati ambapo kinyume kabisa cha mtazamo wako ni kweli, na kwa kutumia dhana zako za kibinafsi katika kujaribu na kumpima Mungu, tayari umemghadhabisha. Hii ni kwa sababu Mungu hafanyi kazi kama unavyofikiria wewe, Naye Mungu hatalishughulikia suala hili kama vile unavyosema Atalishughulikia. Na hivyo basi Nakukumbusha kuwa makini na mwenye hekima katika mtazamo wako katika kila kitu, na ujifunze namna ya kufuata kanuni ya kutembea kwenye njia ya Mungu katika mambo yote—kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Lazima uimarisha uelewa dhabiti katika masuala ya mapenzi ya Mungu na mwelekeo wa Mungu; kutafuta watu walio na nuru kuuwasilisha kwako, na kutafuta kwa dhati. Usimwone Mungu wa imani yako kama kicaragosi—kuhukumu kiholela, kufikia hitimisho kiholela, kutomshughulikia

Mungu kwa heshima Anayostahili. Katika mchakato wa wokovu wa Mungu Anapofafanua matokeo yako, bila kujali kama Yeye atakupa rehema, au uvumilivu, au hukumu na kuadibu, mwelekeo Wake kwako wewe unabadilika. Inategemea na mwelekeo wako kwa Mungu, na uelewa wako wa Mungu. Usiache dhana moja ya kupita ya maarifa au uelewa wako katika Mungu kumfafanua Yeye daima. Usisadiki katika Mungu aliyekufa; amini kwa yule aliye hai. Kumbuka hili! Ingawa Nimezungumzia ukweli fulani hapa, ukweli mliohitaji kusikia, kwa mujibu wa hali yenu ya sasa na kimo chenu cha sasa, Sitatoa mahitaji yoyote makubwa zaidi ili nisije nikaiondoa shauku yenu. Kufanya hivyo kutajaza mioyo yenu na huzuni na simanzi, na kuwafanya nyinyi kuhisi masikitiko mengi mno kwa Mungu. Badala yake Natumai kwamba mnaweza kutumia upendo wa Mungu katika mioyo yenu, na kutumia mwelekeo ambao ni wa heshima kwa Mungu wakati mnapotembea kwenye njia iliyo hapo mbele. Usimalizie suala la jinsi ya kushughulikia imani ya Mungu kwa kubahatisha. Lishughulikie kama mojawapo ya maswali makubwa zaidi yaliyopo. Liwekeni kwenye mioyo yenu, litieni kwenye matendo, unganeni nalo kupitia kwa maisha halisi—msikubaliane nalo kwa maneno pekee. Kwani hili ni suala la uzima na mauti, na ndilo ambalo litaamua hatima yako. Usilichukulie kama mzaha, kama mchezo wa mtoto! Baada ya kuwaambia maneno haya leo, Najiuliza mavuno ya uelewa yamekuwa nini katika akili zenu? Kunayo maswali yoyote ambayo ungependa kuuliza kuhusu kile Nilichokisema leo?

Ingawa mada hizi ni mpya kidogo, na zimeondolewa kidogo kutoka kwenye mitazamo yenu na kile ambacho kwa kawaida mnafuatilia na kutilia maanani, Nafikiria kwamba baada ya mada hizi kuwasilishwa kwa kipindi cha muda, mtaimarisha uelewa mzuri wa kila kitu Nilichosema hapa. Kwa sababu hizi ni mada mpya, mada ambazo hujawahi kufikiria awali, Ninatumai kwamba hazitaongezea mzigo kwako. Ninaongea maneno haya leo si kwa sababu ya kuwatishia nyinyi, wala Sijaribu kukushughulikia wewe; badala yake, nia Yangu ni kukusaidia kuelewa ukweli wa hoja. Kwa vyovyote vile, kunao umbali kati ya wanadamu na Mungu. Ingawa binadamu anaamini katika Mungu, hajawahi kumwelewa Mungu; hajawahi kujua mitazamo ya Mungu. Binadamu pia hajawahi kuwa na shauku katika kuujali mwelekeo wa Mungu. Badala yake, amesadiki kwa kutojua, ameendelea mbele kwa kutojua na amekosa kumakinika katika maarifa na uelewa wake wa Mungu. Hivyo basi Nahisi mshawasha wa kuyafumbua masuala haya kwa niaba yenu na kuwasaidia kuelewa huyu Mungu unayemsadiki hasa ni Mungu wa aina gani; kile Anachofikiria; mwelekeo Wake ni nini katika kushughulikia Kwake kwa watu wa aina tofauti; uko mbali kiasi gani kukamilisha mahitaji Yake; na tofauti iliopo kati ya hatua zako na kiwango anachohitaji Yeye. Shabaha katika kujua kwako haya ni kuwapa kigezo cha kupimia kwenye mioyo yenu ambacho mtaweza kupimia dhidi ya na kujua barabara mnayotembelea imewaelekeza katika mavuno aina gani, kile ambacho hamjapata kwenye barabara hii, na

sehemu zile ambazo hamjajihusisha kwazo. Wakati mnawasiliana miongoni mwa nyinyi wenyewe, kwa kawaida mnazungumzia mada chache zinazungumziwa kwa kawaida; upana huo wa kazi ni mwembamba, na maudhui ni ya juujuu sana. Kunao umbali, nafasi, kati ya kile ambacho mnazungumzia na nia za Mungu, katikati ya mazungumzo yenu na upana na kiwango cha mahitaji ya Mungu. Kuendelea hivi baada ya muda kutawafanya kupotoka zaidi na zaidi kutoka kwenye njia ya Mungu. Mnayachukua tu maneno yaliyopo kutoka kwa Mungu na kuyageuza kuwa vifaa vya kuabudu, kuwa kaida za dini na utaratibu. Hayo tu ndiyo maana yake! Kwa hakika, Mungu hana nafasi kamwe katika mioyo yenu, na Mungu hajawahi kuipata mioyo yenu. Baadhi ya watu hufikiria kwamba kumjua Mungu ni vigumu sana—huu ndio ukweli. Ni vigumu! Kama watu wataambiwa kutekeleza wajibu wao na kuhakikisha kwamba mambo yanatendeka kwa nje, kama wataulizwa kutia bidii, basi watu watafikiria kwamba kusadiki Mungu ni jambo rahisi sana, kwa sababu haya yote yanapatikana katika ule upana wa uwezo wa binadamu. Ilhali punde tu mada hizo zinaposonga kuelekea kwenye maeneo ya nia za Mungu na mwelekeo wa Mungu kwa binadamu, basi mambo yanapata kuwa magumu zaidi kwa watu wote. Hiyo ni kwa sababu yote haya yanahusisha uelewa wa ukweli na kuingia kwao katika uhalisia; bila shaka kuna kiwango cha ugumu. Lakini baada ya wewe kuingia kupitia mlango wa kwanza, baada ya wewe kuanza kuingia ndani yake, mambo yanaanza kuwa rahisi na rahisi kwa utaratibu.

Sehemu ya Mwanzo ya Kumcha Mungu ni Kumtendea Kama Mungu

Mtu fulani amelizua swali hivi punde: Inakuwaje kwamba tunajua zaidi kuhusu Mungu kuliko alivyojua Ayubu, ilhali bado hatuwezi kumcha Mungu? Tuliligusia swala hili hapo awali kidogo, sivyo? Kwa hakika, kiini halisi cha swali hili kimeweza pia kuzungumziwa awali kwamba ingawa Ayubu hakumjua Mungu wakati huo, alimshughulikia Yeye kama Mungu, na kumchukulia Yeye kama Bwana wa mambo yote mbinguni na nchini. Ayubu hakumchukulia Mungu kuwa adui. Badala yake, alimwabudu Yeye kama Muumba wa viumbe vyote. Watu siku hizi wanampinga Mungu sana kwa nini? Kwa nini hawawezi kumcha Mungu? Sababu moja ni kwamba wamepotoshwa pakubwa na Shetani. Wakiwa na asili yao ya kishetani ikiwa imekita mizizi ndani, watu wanageuka na kuwa adui wa Mungu. Hivyo basi, hata ingawa wanasadiki katika Mungu na kumtambua Mungu, bado wanaweza kumpinga Mungu na kujiweka katika nafasi ya upinzani na Yeye. Hili linaamuliwa na asili ya binadamu. Sababu nyingine ni kwamba ingawa watu wanasadiki Mungu, hawamchukulii Yeye tu kama Mungu. Badala yake, wanamchukulia Mungu kuwa ndiye anayempinga binadamu, wakimwona Yeye kuwa adui wa binadamu, na hawawezi kupatanishwa na Mungu. Ni rahisi hivyo. Je, jambo hili halikuzungumziwa kwenye kikao cha awali? Hebu fikiria: Hiyo ndiyo sababu? Ingawa unayo maarifa kidogo ya Mungu, maarifa haya hasa ni nini? Haya siyo yale kila mtu anazungumzia?

Haya si yale ambayo Mungu alikuambia? Unajua tu zile dhana za kinadharia na kifalsafa; umewahi kupitia dhana halisi ya Mungu? Je, unayo maarifa ya kibinafsi? Je, unayo maarifa na uzoefu wa kimatendo? Kama Mungu asingekuambia, ungelijua hili? Maarifa yako katika nadharia hayawakilishi maarifa halisi. Kwa ufupi, bila kujali ni kiwango kipi unachojua na ni vipi ulivyokijua hatimaye, kabla ya wewe kufikia uelewa halisi wa Mungu, Mungu ndiye adui wako, na kabla ya wewe kumshughulikia Mungu hivyo, Amewekwa kuwa mpinzani wako, kwani wewe ni mfano halisi wa Shetani.

Unapokuwa pamoja na Kristo, pengine unaweza kumhudumia kwa milo mitatu kwa siku, pengine kumhudumia Yeye kwa chai, kuyashughulikia mahitaji Yake ya maisha, ni kana kwamba unamshughulikia Kristo kama Mungu. Kila wakati jambo linapofanyika, mitazamo ya watu siku zote inakuwa kinyume cha mtazamo wa Mungu. Siku zote wanashindwa kuelewa mtazamo wa Mungu, na wanashindwa kuukubali. Ingawa watu wanaweza kupatana na Mungu juujuu, hii haimaanishi kwamba wanalingana na Yeye. Punde tu jambo linapofanyika, ukweli wa kutotii kwa binadamu unaibuka, na kuthibitisha ukatili uliopo kati ya binadamu na Mungu. Ukatili huu si wa Mungu kumpinga binadamu; si Mungu kutaka kuwa katili kwa binadamu, na si Mungu kumweka binadamu katika upinzani na kumshughulikia binadamu hivyo. Badala yake, ni hali ya upinzani huu wa kiini halisi kwa Mungu ambao unajificha katika mapenzi ya kibinafsi ya binadamu, na katika akili ya kutofahamu ya binadamu. Kwa sababu binadamu anachukulia kila kitu kinachotoka kwa Mungu kama kifaa cha utafiti wake, mwitikio wake kwa hiki ambacho kinatoka kwa Mungu na kile ambacho kinamhusisha Mungu ni, zaidi ya yote, kukisia, na kushuku, na kisha haraka sana kuingia katika mwelekeo ambao unakinzana na Mungu, na unapingana na Mungu. Baada ya hapo, binadamu atachukua hali hizi za moyo za kimyakimya na kuzua mjadala na Mungu au kushindana na Mungu hadi kufikia kiwango ambacho atatia shaka kama Mungu wa aina hii anastahili kufuatwa. Licha ya hoja kwamba urazini wa binadamu unamwambia asiendele hivi, bado atachagua kufanya hivyo licha ya kutotaka kufanya hivyo, kiasi kwamba ataendelea bila kusita hadi mwisho. Kwa mfano, ni nini mwitikio wa kwanza kwa baadhi ya watu wanaposikia uvumi fulani au matusi fulani kumhusu Mungu? Mwitikio wa kwanza ni: Sijui kama uvumi huu ni kweli au la, kama upo ama haupo, hivyo basi nitasubiri na kuona. Kisha wanaanza kutafakari: Hakuna njia ya kuthibitisha haya; ipo kweli? Uvumi huu ni kweli au la? Ingawa mtu huyu haonyeshi juujuu, moyo wake tayari umeanza kutia shaka, tayari umeanza kumkataa Mungu. Ni nini kiini halisi cha aina hii ya mwelekeo, aina hii ya mtazamo? Je huu si usaliti? Kabla ya wao kukumbwa na suala, huwezi kuona mtazamo wa mtu huyu ni nini—yaonekana ni kana kwamba wao hawakinzani na Mungu, ni kama hawamchukulii Mungu kuwa adui. Hata hivyo, punde wanapokumbwa na suala hilo, wanasimama mara moja na Shetani na kumpinga Mungu. Hali hii inapendekeza nini? Inapendekeza kwamba binadamu na Mungu

wanapingana! Si kwamba Mungu anamchukulia binadamu kama adui, lakini kwamba kile kiini halisi chenyewe cha binadamu ni kikatili kwa Mungu. Haijalishi ni kwa muda mrefu vipi ambapo mtu humfuata Mungu, ni kiwango kipi anacholipia; haijalishi vipi ambavyo mtu anamsifu Mungu, anavyojihifadhi dhidi ya kumpinga Mungu, hata akijisihi kumpenda Mungu, hatawahi kufaulu kumshughulikia Mungu kama Mungu. Si hali hii inaamuliwa na kiini halisi cha mwanadamu? Kama Utamshughulikia kama Mungu, unaweza kwa kweli kusadiki kwamba Yeye ni Mungu, unaweza bado kuwa na shaka lolote kwake Yeye? Bado kunaweza kuwa na maswali yoyote yanayomhusu Yeye katika moyo wako? Hakuwezi. Mitindo ya ulimwengu huu ni miovu kweli, na wanadamu wa kizazi hiki pia, hivyo, inawezekanaje kwamba huna fikira zozote kuzihusu? Wewe mwenyewe umejaa uovu, hivyo inakuwaje kwamba huna fikira zozote kuhusu hayo? Ihali uvumi mchache tu, matusi fulani yanaweza kusababisha dhana kubwa mno kumhusu Mungu, zinaweza kuleta mawazo mengi mno, hali inayoonyesha vile ambavyo kimo chako kilivyo bado kichanga! “Mnong’ono” tu wa mbu wachache, nzi wachache wabaya, hilo tu ndilo linalokupotosha? Huyu ni mtu wa aina gani? Je, unajua anachofikiria Mungu kuhusu mtu wa aina hii? Mwelekeo wa Mungu kwa hakika uko wazi sana kuhusiana na ni vipi Anavyowashughulikia watu hawa. Ni kwa sababu tu kwamba ushughulikiaji wa Mungu kwa watu hawa ni kuwapuuza—mwelekeo Wake ni kutowatilia maanani, na kutomakinikia watu hawa wasiojua. Kwa nini hivyo? Kwa sababu katika moyo Wake Hakuwahi kupangilia kuhusu kupata watu hao ambao wameahidi kuwa wakatili kwake Yeye hadi mwisho, na ambao hawajawahi kupangilia kutafuta njia ya uwiano na Yeye. Pengine maneno haya Niliyoyaongea yamewaumiza watu wachache. Kwa kweli, mko radhi kuniruhusu Mimi kuwadhuru siku zote namna hii? Bila kujali kama mko radhi au la, kila kitu Ninachosema ni ukweli! Kama siku zote Ninawadhuru namna hii, siku zote Nafichua makovu yenu, je, itaathiri taswira za majivuno kuhusu Mungu katika mioyo yenu? (Haitaathiri.) Ninakubali kwamba haitaathiri kwani kwa ufupi hakuna Mungu katika mioyo yenu. Yule Mungu wa majivuno anayepatikana ndani ya mioyo yenu, yule mnayemtetea kwa dhati na kulinda, kwa ufupi si Mungu. Badala yake ni ndoto ya kufikiria kwa binadamu; kwa ufupi haipo. Hivyo basi ni bora zaidi kama Nitafichua jibu la kitendawili hiki. Je, huu si ukweli wote? Mungu halisi hatokani na kufikiria kwa binadamu. Natumai kwamba nyote mnaweza kukabiliana na uhalisia huu, na utawasaidia katika maarifa yenu ya Mungu.

Wale Watu Wasiotambuliwa na Mungu

Kunao baadhi ya watu ambao imani yao haijawahi kutambuliwa katika moyo wa Mungu. Kwa maneno mengine, Mungu hatambui kwamba watu hawa ni wafuasi Wake, kwa sababu Mungu haisifu imani yao. Kwa watu hawa, haijalishi wamemfuata Mungu kwa miaka mingapi, mawazo na mitazamo yao haijawahi kubadilika. Wao ni kama wasioamini, wanatii kanuni na

njia ambayo wasioamini wanafanya mambo yao, kutii sheria zao za kusalia na imani. Hawakuwahi kukubali neno la Mungu kama maisha yao, hawakuwahi kusadiki kwamba neno la Mungu ni ukweli, hawakuwahi kunuia kukubali wokovu wa Mungu, na hawakuwahi kutambua Mungu kama Mungu wao. Wanachukulia kusadiki Mungu kuwa uraibu fulani wa wanagenzi, wakashughulikia Mungu kama riziki ya kiroho, hivyo basi hawafikirii kwamba ipo thamani ya kujaribu na kuelewa tabia ya Mungu, au kiini halisi cha Mungu. Unaweza kusema kwamba kila kitu kinacholingana na Mungu wa kweli hakihusiani kwa vyovyote vile na watu hawa. Hawana hamu yoyote, na hawawezi kusumbuliwa kutilia maanani. Hii ni kwa sababu ndani kabisa ya mioyo yao kunayo sauti ya nguvu ambayo siku zote inawaambia: Mungu haonekani na hagusiki, na Mungu hayupo. Wanasadiki kwamba kujaribu kumwelewa Mungu wa aina hii hakutastahili jitihada zao; itakuwa sawa na wao kujidanganya. Wao wanaamini tu kwa kumtambua Mungu kwa maneno tu bila kuchukua msimamo wowote halisi au kujiweka ndani yao kupitia vitendo halisi, wao wanakuwa werevu sana. Mungu anachukulia vipi watu kama hawa? Anawachukulia kuwa wasioamini. Baadhi ya watu huuliza: “Je, wasioamini wanaweza kulisoma neno la Mungu? Je, wanaweza kutekeleza wajibu wao? Je, wanaweza kuyasema maneno haya: ‘Nitaishi kwa ajili ya Mungu?’” Kile ambacho binadamu huona mara nyingi ni maonyesho ya juujuu tu ya watu, na wala si kiini chao halisi. Ilhali Mungu haangalii maonyesho haya ya juujuu; Yeye huona tu kiini chao halisi cha ndani. Hivyo basi, Mungu anao mwelekeo wa aina hii, ufafanuzi wa aina hii, kwa watu kama hawa. Kuhusiana na kile ambacho watu hawa husema: “Kwa nini Mungu hufanya hivi? Kwa nini Mungu hufanya vile? Siwezi kuelewa haya; siwezi kuelewa yale; haya hayaingiliani na fikira za binadamu; Lazima unielezee haya; ...” Jibu langu ni: Inahitajika kuelezea suala hili kwako? Je, suala hili lina chochote kuhusiana na wewe? Unafikiria wewe ni nani? Ulitokea wapi? Umefuzu kumwelekeza Mungu? Je, unamwamini Yeye? Je, Anatambua imani yako? Kwa sababu imani yako haina chochote kuhusiana na Mungu, matendo Yake yana uhusiano gani na wewe? Hujui pale ulipo katika moyo wa Mungu, ilhali umefuzu kuzungumza na Mungu?

Maneno ya Maonyo

Hamhisi vibaya baada ya kusikia matamshi haya? Ingawa huenda msiwe radhi kusikiliza maneno haya, au msiwe radhi kuyakubali, yote ni uhakika. Kwa sababu awamu hii ya kazi ni ya Mungu kutenda, kama hujali nia za Mungu, hujali mwelekeo wa Mungu na huelewi kiini halisi na tabia ya Mungu, basi hatimaye wewe ndiwe utakayekosa kufaidi. Msiyalaumu maneno yangu kwa kuwa magumu kusikiliza, na msiyalaumu kwa kupunguza majivuno ya shauku yenu. Mimi naongea ukweli; na wala Sinuii kuwavunja moyo. Haijalishi ni nini Ninachowauliza ninyi, na haijalishi ni vipi mnavyohitajika kukifanya, Ninatumai kwamba mtatembelea njia sahihi, na ninatumai kwamba mtafuata njia ya Mungu na wala msipotoke katika njia hii. Kama hutaendelea

kulingana na neno la Mungu, na hufuati njia Yake, basi hakutakuwa na shaka kwamba unaasi dhidi ya Mungu na umepotea kutoka kwa njia sahihi. Hivyo basi Nahisi kwamba yapo masuala fulani ambayo lazima Niwabainishie, na kuwafanya kusadiki dhahiri shairi, waziwazi, bila ya tone la mashaka na kuwasaidia waziwazi kujua mwelekeo wa Mungu, nia za Mungu, namna Mungu anavyomfanya binadamu kuwa mtimilifu, na ni kwa njia gani Yeye Hupanga matokeo ya binadamu. Endapo kutakuwa na siku ambayo hutaweza kuanza katika njia hii, basi Sitahitajika kuwajibika kwa vyovyote vile kwa sababu maneno haya tayari yamezungumzwa kwako waziwazi. Kuhusiana na matokeo ya aina tofauti ya watu Mungu Anayo mitazamo tofauti. Anazo njia Zake binafsi za kuwapima, vile vile kama kiwango Chake binafsi cha mahitaji kwao. Kiwango Chake cha kupima matokeo ya watu ni kile ambacho ni chenye haki kwa kila mmoja—hakuna shaka kuhusu hilo. Hivyo basi, woga wa watu fulani hauhitajiki. Je, umepata tulizo la moyo sasa? Ndivyo hivyo kwa leo. Kwaheri!

Oktoba 17, 2013

Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe I

Leo tunawasiliana kuhusu mada muhimu. Hii ni mada ambayo imezungumziwa tangu kuanza kwa kazi ya Mungu mpaka sasa, na inayo umuhimu mkuu kwa kila mtu. Kwa maneno mengine, hili ni suala ambalo kila mmoja atakutana nalo kwenye mchakato wote wa kusadiki kwake katika Mungu na suala ambalo lazima lizungumziwe. Ni suala muhimu, lisiloepukika ambalo mwanadamu hawezi kujitenganisha nalo. Tukizungumzia umuhimu, ni nini kitu muhimu zaidi kwa kila muumini katika Mungu? Baadhi ya watu wanafikiri kwamba kitu muhimu zaidi ni kuyaelewa mapenzi ya Mungu; baadhi wanasadiki ni muhimu zaidi kula na kunywa maneno ya Mungu; baadhi wanahisi kitu muhimu zaidi ni kujijua wenyewe; wengine wanayo maoni kwamba kitu muhimu zaidi ni kujua namna ya kupata wokovu kupitia kwa Mungu, namna ya kumfuata Mungu, na namna ya kuyatimiza mapenzi ya Mungu. Tutayaweka masuala haya yote pembeni kwa leo. Hivyo basi ni nini tunachozungumzia? Tunazungumzia mada kuhusu Mungu. Je, hii ndiyo mada muhimu zaidi kwa kila mtu? Maudhui ya mada kuhusu Mungu ni yapi? Bila shaka, mada hii haiwezi kamwe kutenganishwa na tabia ya Mungu, kiini cha Mungu na kazi ya Mungu. Hivyo leo, hebu tuzungumzie “Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe.”

Tangu wakati binadamu walipoanza kumsadiki Mungu, wamekuwa wakikutana na mada kama vile kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe. Inapokuja kwa kazi ya Mungu, baadhi ya watu watasema: “Sisi ndio tunaofanyiwa kazi ya Mungu; tunaipitia kila siku, na hivyo basi tumezoeana nayo.” Na kuhusiana na tabia ya Mungu, baadhi ya watu watasema:

“Tabia ya Mungu ni mada tunayoisoma, kuchunguza, na kuzingatia katika maisha yetu yote, hivyo basi tunafaa kuzoeana nayo.” Na kama ni Mungu Mwenyewe, baadhi ya watu watasema: “Mungu Mwenyewe ndiye tunayemfuata, tuliye na imani Kwake, na ndiye tunayemfuata, hivyo tumejuzwa pia kuhusu Yeye.” Mungu hajawahi kukomesha kazi Yake tangu uumbaji, wakati wote huu Ameendelea kuonyesha tabia Yake na kutumia njia mbalimbali kuonyesha neno Lake. Wakati huohuo, hajawahi kusita kujionyesha Yeye Mwenyewe na kiini Chake kwa mwanadamu, akionyesha mapenzi Yake kwa binadamu na kile Anachohitaji kutoka kwa huyo binadamu. Hivyo kutoka katika mtazamo wa moja kwa moja, mada hizi hazifai kuwa za kigeni kwa yeyote yule. Kwa watu wanaomfuata Mungu leo, hata hivyo, Kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe kwa hakika ni mambo ambayo hayajulikani kwao. Kwa nini hali iko hivi? Kwa kadri binadamu anapopitia kazi ya Mungu, anawasiliana pia na Mungu, na kuwafanya kuhisi ni kana kwamba wanaelewa tabia ya Mungu au wanajua sehemu kidogo kuhusu vile inavyofanana. Hivyo basi, binadamu hafikiri kuwa yeye ni mgeni katika kazi ya Mungu au tabia ya Mungu. Badala yake, binadamu anafikiri ni mwenyeji kabisa na Mungu na anaelewa mengi kuhusu Mungu. Lakini kulingana na hali ya sasa, uelewa wa watu wengi kumhusu Mungu umezuiliwa katika kile walichosoma vitabuni, na upana mfinyu wa kile walichopitia wao binafsi, wakiwa wamezuiliwa na kufikiria kwao, na zaidi ya yote, ukiwa umewekewa mipaka ya ukweli wanaoweza kuona kwa macho yao binafsi. Haya yote yapo mbali sana na Mungu Mwenyewe wa kweli. Sasa huu umbali upo “mbali” vipi? Pengine binadamu mwenyewe hana hakika, au pengine binadamu anayo dhana, ana fununu kiasi—lakini kwake Mungu Mwenyewe, uelewa wa binadamu kumhusu Yeye u mbali sana na kiini cha Mungu Mwenyewe wa kweli. Hii ndiyo maana tunahitajika kutumia mada kama “Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe” ili kuwasilisha ujumbe huu hatua kwa hatua na kwa njia mahususi.

Kwa hakika, tabia ya Mungu iko wazi kwa kila mmoja na haijafichwa, kwa sababu Mungu hajawahi kuepuka kimakusudi mtu yeyote na Hajawahi kimakusudi kujaribu kujificha Mwenyewe ili watu wasiweze kumjua Yeye au kumwelewa Yeye. Tabia ya Mungu siku zote imekuwa wazi na siku zote imekuwa ikitazama kila mtu kwa njia ya uwazi. Katika usimamizi wa Mungu, Mungu hufanya kazi Yake akitazama kila mmoja; na kazi Yake ndiyo inafanywa kwa kila mtu. Anapofanya kazi hii, Anafichua bila kusita tabia Yake, huku Akitumia bila kusita kiini Chake na kile Anacho na alichio kuongoza na kukimu kila mmoja. Katika kila enzi na kila awamu, licha ya kama hali ni nzuri au mbaya, tabia ya Mungu siku zote iko wazi kwa kila mtu binafsi, na vile vitu Anavyomiliki na uwepo Wake siku zote viko wazi kwa kila mtu binafsi, kwa njia sawa kwamba maisha Yake yanamtoshelezea mwanadamu kila wakati na bila kusita na kumsaidia mwanadamu. Licha ya haya yote, tabia ya Mungu inabakia fiche kwa baadhi ya watu. Kwa nini iko hivyo? Ni kwa sababu ingawaje watu hawa wanaishi ndani ya kazi ya Mungu na

wanamfuata Mungu, hawajawahi kutafuta kuelewa Mungu au kutaka kumjua Mungu, sikwambii hata kumkaribia Mungu. Kwa watu hawa, kuelewa tabia ya Mungu kunamaanisha mwisho wao wawadia; kwa maanisha karibu wanahukumiwa na kushtakiwa na tabia ya Mungu. Hivyo basi, watu hawa hawajawahi kutamani kuelewa Mungu au tabia Yake, na hawatamani uelewa au maarifa ya kina ya mapenzi ya Mungu. Hawanuii kufahamu mapenzi ya Mungu kupitia ushirikiano wa kimakusudi—wanafurahia tu milele na hawachoki kufanya mambo wanayotaka kuyafanya; kusadiki kwa Mungu wanayetaka kusadiki Kwake; kusadiki kwa Mungu aliyepo tu katika fikira zao, Mungu aliyepo tu katika dhana zao; na kusadiki kwa Mungu asiyeveza kutenganishwa na wao katika maisha yao ya kila siku. Na kwake Mungu Mwenyewe wa kweli, wanapuuza kabisa, hawataki kusikia mambo ya Mungu na hawana tamanio la kumwelewa Yeye, kumtilia maanani Yeye, sembuse kuwa na tamanio la kuwa karibu zaidi na Yeye. Wanayatumia tu maneno ambayo Mungu anayaonyesha ili kuweza kujirembesha, kujiandaa upya. Kwa wao, hilo tayari linawafanya kuwa waumini wenye mafanikio na watu walio na imani kwa Mungu ndani ya mioyo yao. Ndani ya mioyo yao, wanaongozwa na kufikiria kwao, dhana zao, na hata ufasili wao binafsi wa Mungu. Mungu Mwenyewe wa kweli, kwa mkono mwingine, hana chochote kuhusiana na wao. Kwa sababu pindi wanapomwelewa Mungu Mwenyewe wa kweli, kuelewa tabia ya Mungu ya kweli, na kuelewa kile Mungu anacho na alichu, hii inamaanisha kwamba vitendo vyao, imani yao, na yale yote wanayoyafuatilia yatashutumiwa. Na ndiyo maana hawako radhi kukielewa kiini cha Mungu, na ndiyo maana wanasitasita na hawako radhi kutafuta kwa bidii au kuomba kumwelewa zaidi Mungu, kupata kujua zaidi kuhusu mapenzi Yake Mungu, na kuelewa kwa njia bora zaidi tabia ya Mungu. Afadhali Mungu kwao awe kitu kilichotungwa, kitu kisicho na chochote na kisicho dhahiri. Afadhali kwao Mungu awe mtu ambaye yupo hasa vile ambavyo wamemfikiria Yeye, Anayeweza kunyenyekea mbele zao, Asiyeishiwa na ujazo na Anayepatikana siku zote. Wanapotaka kufurahia neema ya Mungu, wanamuomba Mungu kuwa hiyo neema. Wanapohitaji baraka za Mungu, wanamuomba Mungu kuwa baraka hizo. Wanapokabiliwa na dhiki, wanamwomba Mungu kuwatia wao moyo, na kuwa usalama wao. Maarifa ya watu hawa kumhusu Mungu imebakia palepale pa mipaka ya neema na baraka. Uelewa wao wa kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, na Mungu umezuiliwa pia na kufikiria kwao na vilevile barua na mafundisho ya kidini tu. Lakini wapo baadhi ya watu walio na hamu ya kuielewa tabia ya Mungu, wanaotaka kumwona Mungu Mwenyewe kwa kweli, na kuielewa tabia ya Mungu kwa kweli na kile Anacho na alichu. Watu hawa wanatafuta uhalisia wa ukweli na wokovu wa Mungu na wanatafuta kupokea ushindi, wokovu, na utimilifu wa Mungu. Watu hawa wanaitumia mioyo yao kulisoma neno la Mungu, wanaitumia mioyo yao kuthamini hali na kila mtu, tukio, au kitu ambacho Mungu amewapangia, na kuomba na kutafuta kwa uaminifu. Kile wanachotaka zaidi ni kuyajua mapenzi ya Mungu na kuielewa tabia ya kweli na kiini cha Mungu. Hivi ndivyo ilivyo ili wasiweze tena kumkosea Mungu, na kupitia kwa

mambo waliyoyapitia, waweze kuona upendo zaidi wa Mungu na upande Wake wa kweli. Iko hivyo pia ili Mungu halisi na wa kweli ataweza kuwepo ndani ya mioyo yao, na ili Mungu atakuwa na nafasi katika mioyo yao, kiasi cha kwamba hawatakuwa wakiishi tena miongoni mwa kufikiria, dhana, au hali ya kuyaepuka mambo. Kwa watu hawa, sababu inayowafanya kuwa na tamania kuu la kuielewa tabia ya Mungu na kiini Chake ni kwa sababu tabia ya Mungu na kiini Chake ni mambo ambayo mwanadamu anaweza kuyahitaji wakati wowote katika uzoefu wao, mambo yanayojaza uhai katika maisha yao yote walioishi. Pindi wanapoelewa tabia ya Mungu, wataweza kumheshimu sana kwa njia bora zaidi, kushirikiana kwa njia bora zaidi na kazi ya Mungu, na kuyaweka zaidi katika fikira mapenzi ya Mungu na kutekeleza wajibu wao kwa njia bora zaidi wakitumia uwezo wao. Hawa ndio watu wa aina mbili inapokuja katika mielekeo yao kwa tabia ya Mungu. Watu wa aina ya kwanza hawataki kuielewa tabia ya Mungu. Ingawaje wanasema wanataka kuielewa tabia ya Mungu, kupata kumjua Mungu Mwenyewe, kuona kile Mungu anacho na alichio, na kushukuru kwa dhiti mapenzi ya Mungu, ndani yao kabisa wanaona afadhali Mungu asikuwepo. Ni kwa sababu watu wa aina hii wanakosa kumtii Mungu kila wakati na wanampinga; wanapigana na Mungu kwa sababu ya vyeo vilivyo ndani ya mioyo yao na mara nyingi wanashuku na hata kukataa uwepo wa Mungu. Hawataki kuruhusu tabia ya Mungu au kuacha Mungu mwenyewe wa kweli kumiliki mioyo yao. Wanataka tu kutosheleza matamania, kufikiria, na maono yao binafsi. Hivyo basi, watu hawa wanaweza kumsadiki Mungu, kumfuata Mungu, na hata wanaweza kutupilia mbali familia na kazi zao kwa sababu Yake Yeye, lakini hawasitishi njia zao za maovu. Baadhi yao hata huiba au kubadhiri sadaka au kumlaani Mungu kisirisiri, huku wengine wakiweza kutumia vyeo vyao kushuhudia mara kwa mara kuhusu wao wenyewe, kujiongezea zaidi umaarufu wao, na kushindana na Mungu kwa ajili ya watu na hadhi. Wanatumia mbinu na njia mbalimbali kuwafanya watu kuwaabudu, kujaribu mara kwa mara kuwa na ufuasi mkubwa wa watu na kutaka kuwadhibiti watu hao. Baadhi hata hupotosha kimakusudi watu na kuwafanya kufikiria kwamba wao ni Mungu ili waweze kuchukuliwa kama Mungu. Hawawezi katu kuwaambia watu kwamba wamepotoshwa, kwamba pia wao wamepotoka na wana kiburi, na hivyo basi hawafai kuwaabudu, na kwamba haijalishi watafanya vyema kiasi kipi, haya yote ni kutokana na utukuzaji wa Mungu na kile wanachostahili kufanya kwa kweli. Kwa nini hawasemi mambo haya? Kwa sababu wana hofu kuu ya kupoteza nafasi yao ndani ya mioyo ya watu. Hii ndiyo maana watu kama hao hawamtukuzi Mungu katu na katu hawamshuhudii Mungu, kwani hawajawahi kujaribu kumwelewa Mungu. Wanaweza kumjua Mungu kama hawamwelewi? Haiwezekani! Hivyo, ingawa maneno katika mada “Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe” yanaweza kuwa rahisi, maana yao ni tofauti kwa kila mmoja. Kwa mtu anayekosa kumtii Mungu mara kwa mara, na anampinga Mungu na ni mkatili kwa Mungu, maneno hayo yanabashiri shutuma; ilhali mtu anayefuatilia uhalisi wa kweli na mara nyingi anakuja mbele ya

Mungu kutafuta mapenzi ya Mungu atayachukulia maneno hayo kama kawaida yake. Hivyo kuwa wale walio miongoni mwenu, wanaposikiza mazungumzo ya tabia ya Mungu na kazi ya Mungu, wanaanza kuumwa na kichwa, mioyo yao inajaa upinzani, na wanakuwa katika hali isiyo na utulivu kabisa. Lakini kuna wengine miongoni mwenu wanaofikiria: Mada hii ndiyo hasa Ninayohitaji, kwa sababu mada hii ni yenye manufaa sana kwangu. Ni sehemu ambayo haiwezi kukosekana katika uzoefu wangu wa maisha; ni swali ambalo halijapata jibu bado, msingi wa imani kwa Mungu, na jambo ambalo mwanadamu hawezi kufikiria kuliacha. Kwenu nyote, mada hii inaweza kuonekana kuwa karibu na mbali, isiyojulikana ilhali inayozoeleka. Lakini haijalishi ni nini, hii ni mada ambayo kila mmoja lazima aisikilize, aijue, na lazima aielewe. Haijalishi ni vipi utakavyoishughulikia, haijalishi ni vipi utakavyoiangalia au utakavyoipokea, lakini umuhimu wa mada hii huwezi kupuuzwa.

Mungu amekuwa akifanya kazi Yake tangu Awaumbe wanadamu. Mwanzoni, ilikuwa kazi rahisi sana, lakini licha ya urahisi wake, ingali ilikuwa na maonyesho ya kiini na tabia ya Mungu. Ingawa kazi ya Mungu sasa imepandishwa daraja, na Yeye akitia kiwango kikubwa mno cha kazi thabiti kwa kila mmoja anayemfuata Yeye, na kuonyesha kiwango kikubwa cha neno Lake, kuanzia mwanzo hadi sasa, nafsi ya Mungu imekuwa ikifichwa kutoka kwa mwanadamu. Ingawaje amekuwa mwili mara mbili, kuanzia wakati wa simulizi za biblia hadi kwa siku za kisasa, nani amewahi kuona nafsi halisi ya Mungu? Kutokana na uelewa wenu, yupo mtu amewahi kuona nafsi halisi ya Mungu? La. Hakuna aliyewahi kuona nafsi halisi ya Mungu, kumaanisha hakuna aliyewahi kuona nafsi ya kweli ya Mungu. Hili ni jambo ambalo kila mmoja anakubaliana nalo. Hivi ni kusema, nafsi halisi ya Mungu, au Roho wa Mungu, amefichwa kutoka kwa binadamu wote, wakiwemo Adamu na hawa, ambao Aliwaumba, na akiwemo Ayubu mwenye haki, ambaye alikuwa Amemkubali. Hata wao hawakuona nafsi halisi ya Mungu. Lakini kwa nini Mungu anaficha kimakusudi nafsi Yake halisi? Baadhi ya watu husema: “Mungu anaogopa kuwaogofya watu.” Wengine husema: “Mungu huficha nafsi Yake halisi kwa sababu binadamu ni mdogo sana na Mungu ni mkubwa sana; wanadamu hawaruhusiwi kumwona Yeye, la sivyo watakufa.” Wapo pia wale wanaosema: “Mungu ameshughulika sana akisimamia kazi Yake kila siku, huenda Asiwe na muda wa kuonekana na kuruhusu watu kumwona Yeye.” Haijalishi ni nini mnachosadiki, Ninayo hitimisho hapa. Hitimisho hilo ni nini? Ni kwamba Mungu hataki hata watu kuona nafsi Yake halisi. Akiwa amefichwa kutoka kwa binadamu ni kitu ambacho Mungu anafanya kimakusudi. Kwa maneno mengine, ni nia ya Mungu kwa watu kutoona nafsi Yake halisi. Hili linafaa kuwa wazi kwa wote sasa. Kama Mungu hajawahi kuonyesha nafsi Yake kwa yeyote, basi mnafikiria nafsi ya Mungu ipo? (Ipo.) Bila shaka ipo. Uwepo wa nafsi ya Mungu haupingiki. Lakini kuhusu nafsi ya Mungu ni kubwa vipi au inafanana vipi, haya ni maswali ambayo mwanadamu anafaa kuchunguza? La. Jibu ni la.

Kama nafsi ya Mungu si mada ambayo tunafaa kuchunguza, basi ni swali lipi ambalo tunafaa kuchunguza? (Tabia ya Mungu.) (Kazi ya Mungu.) Kabla hatujaanza kuwasiliana mada hii rasmi, hata hivyo, hebu turudi katika kile tulichokuwa tukikizungumzia muda mfupi uliopita: Kwa nini Mungu hajawahi kuonyesha nafsi Yake kwa mwanadamu? Kwa nini Mungu anaficha kimakusudi nafsi Yake kutoka kwa mwanadamu? Kunayo sababu moja tu, nayo ni: Ingawaje binadamu aliyeumbwa amepitia miaka elfu na elfu ya kazi ya Mungu, hakuna hata mtu mmoja anayejua kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, na kiini cha Mungu. Watu kama hao, mbele ya macho ya Mungu, ni upinzani kwake Yeye, na Mungu hatajionyesha kwa watu walio wakatili kwake Yeye. Hii ndiyo sababu ya pekee mbona Mungu hajawahi kumwonyesha binadamu nafsi Yake na ndiyo sababu anaikinga yeye kimakusudi nafsi Yake dhidi yao. Sasa mnaelewa kuhusu umuhimu wa kujua tabia ya Mungu?

Tangu kuwepo kwa usimamizi wa Mungu, siku zote amejitolea kabisa katika kutekeleza kazi Yake. Licha ya kuficha nafsi Yake kutoka kwao, siku zote Amekuwa katika upande wa binadamu, akiwafanyia kazi, akionyesha tabia Yake, akiongoza binadamu wote na kiini Chake, na kufanya kazi Yake kwa kila mmoja kupitia nguvu Zake, hekima Yake, na mamlaka Yake, hivyo akiileta Enzi ya Sheria, Enzi ya Neema, na sasa Enzi ya Ufalme katika uwepo. Ingawaje Mungu huificha nafsi Yake kutoka kwa binadamu, tabia Yake, uwepo Wake na miliki Yake, na mapenzi Yake kwa binadamu yanafichuliwa bila wasiwasi wowote kwa binadamu kwa minajili ya kuona na kupitia hali hiyo. Kwa maneno mengine, ingawaje binadamu hawawezi kumwona au kumgusa Mungu, tabia na kiini cha Mungu ambacho binadamu wamekuwa wakigusana nacho ni maonyesho kabisa ya Mungu Mwenyewe. Je, hayo si kweli? Licha ya ni mbinu gani au ni kutoka katika mtazamo gani Mungu hufanya kazi Yake, siku zote Anawatendeakaribisha watu kulingana na utambulisho Wake wa kweli, akifanya kile ambacho Anafaa kufanya na kusema kile Anachofaa kusema. Haijalishi ni nafasi gani Mungu anazungumzia kutoka—Anaweza kuwa amesimama kwenye mbingu ya tatu, au amesimama akiwa mwili Wake, au hata kama mtu wa kawaida—siku zote Anaongea kwa binadamu kwa moyo Wake wote na kwa akili Zake zote, bila uongo na bila ufichaji wowote. Wakati Anapotekeleza kazi Yake, Mungu huonyesha neno Lake na tabia Yake, na huonyesha kile Anacho na alichu, bila kuficha chochote. Anamwongoza mwanadamu na maisha Yake na uwepo Wake na miliki yake. Hivi ndivyo binadamu alivyoishi katika Enzi ya Sheria—enzi asilia ya binadamu—akiongozwa na Mungu asiyeonekana na asiyeagusika.

Mungu alipata mwili kwa mara ya kwanza baada ya Enzi ya Sheria, hali ya kupata mwili iliyodumu kwa miaka thelathini na tatu na nusu. Kwa mwanadamu, miaka thelathini na mitatu na nusu ni muda mrefu? (Si mrefu sana.) Kwa sababu urefu wa maisha ya mwanadamu ni mirefu kuliko miaka thelathini na fulani, huu si muda mrefu kwa mwanadamu. Lakini kwa Mungu

mwenye mwili, miaka hii thelathini na mitatu na nusu ilikuwa mirefu mno. Aligeuka na kuwa mtu—mtu wa kawaida aliyetekeleza kazi na agizo la Mungu. Hii ilimaanisha kwamba lazima angefanya kazi ambayo mtu wa kawaida asingeweza kufanya, huku akivumilia mateso ambayo binadamu wa kawaida hawezi kuvumilia. Kiwango cha mateso aliyovumilia Bwana Yesu katika Enzi ya Neema, kuanzia mwanzo wa kazi Yake hadi wakati Aliposulubishwa kwenye msalaba, huenda kisiwe ni kitu watu wa leo wangeweza kushuhudia wao binafsi, lakini mnaweza angaa kutambua kiasi kupitia hadithi zilizo kwenye Biblia? Licha ya ni maelezo mangapi yaliyopo kwenye ukweli huu uliorekodiwa, kwa ujumla, kazi ya Mungu katika kipindi hiki kilijaa ugumu na mateso. Kwa mwanadamu aliyepotoka muda wa miaka thelathini na mitatu na nusu si mrefu; mateso kidogo si jambo la kutisha. Lakini kwa Mungu mtakatifu asiye na doa, ambaye lazima avumilie dhambi zote za binadamu, na kula, kulala na kuishi na watenda dhambi, maumivu haya ni mengi mno. Yeye ndiye Muumba, Bwana wa viumbe vyote na Mtawala wa vitu vyote, lakini Alipokuja duniani alilazimika kuvumilia unyanyasaji na ukatili wa wanadamu waliopotoka. Ili kuikamilisha kazi Yake na kuokoa binadamu kutoka kwa taabu, Alilazimika kushutumiwa na binadamu, na kuvumilia dhambi za wanadamu wote. Kiwango cha mateso aliyopitia hakiwezi kwa kweli kueleweka au kutambulika na watu wa kawaida. Mateso haya yanawakilisha nini? Yanawakilisha Mapenzi ya Mungu kwa wanadamu. Yanasimamia udhalilishaji Alioteseka na gharama Aliyolipia kwa sababu ya wokovu wa binadamu, kukomboa dhambi zake, na kukamilisha awamu hii ya kazi Yake. Yanamaanisha binadamu angekombolewa kutoka katika msalaba na Mungu. Hii ndiyo gharama iliyolipwa kwa damu, kwa maisha, gharama ambayo viumbe walioumbwa hawawezi kumudu. Ni kwa sababu Anacho kiini cha Mungu na Amejhami na kile Mungu anacho na alichu, ndiyo maana Anaweza kuvumilia aina hii ya mateso na aina hii ya kazi. Hili ni jambo ambalo hakuna kiumbe aliyeumbwa anaweza kufanya badala Yake. Hii ni kazi ya Mungu katika Enzi ya Neema na ufunuo wa tabia Yake. Je, hii inafichua chochote kuhusu kile Mungu anacho na alichu? Je, wanadamu wanastahili kuijua?

Katika enzi hiyo, japokuwa mwanadamu hakuiona nafsi ya Mungu, alipokea sadaka ya Mungu dhidi ya dhambi zake na akakombolewa kutoka kwenye msalaba na Mungu. Huenda mwanadamu awe amezoeana na kazi aliyofanya Mungu katika Enzi ya Neema, lakini yupo yeyote aliyezoeana na tabia na mapenzi yalionyeshwa na Mungu katika kipindi hiki? Binadamu anajua tu kuhusu maudhui ya kazi ya Mungu katika enzi tofauti katika vipindi mbalimbali, au anajua hadithi zinazohusiana na Mungu zilizofanyika kwa wakati mmoja na ule Mungu alikuwa akitekeleza kazi Yake. Maelezo haya na hadithi ni kwa ukweli zaidi taarifa fulani tu au hadithi za kumbukumbu kuhusu Mungu na vyote hivi havina chochote kuhusiana na tabia na kiini cha Mungu. Hivyo haijalishi ni hadithi ngapi watu wanajua kuhusu Mungu, haimaanishi kwamba wanao uelewa wa kina na maarifa kuhusu tabia ya Mungu au kiini Chake. Kama vile katika Enzi

ya Sheria, ingawaje watu kutoka Enzi ya Neema walikuwa wamepitia mtagusano wa karibu sana na wa kikweli na Mungu wa mwili, maarifa yao kuhusu Mungu na kiini cha Mungu yalikuwa kweli mambo yasiyokuwepo.

Katika Enzi ya Ufalme, Mungu akawa mwili tena, kwa njia sawa na ile Aliyotumia mara ya kwanza. Katika kipindi hiki cha kazi, Mungu angali anaonyesha bila kusita neno Lake, anafanya kazi anayofaa kufanya na kuonyesha kile Anacho na alichio. Wakati huohuo, Anaendelea kuvumilia na kustahili na kutotii na kutojua kwa binadamu. Je, Mungu hafichui kila wakati tabia Yake na kuonyesha mapenzi yake katika kipindi hiki cha kazi pia? Hivyo basi, kuanzia uumbaji wa binadamu hadi sasa, tabia ya Mungu, nafsi Yake na miliki Zake, na mapenzi Yake, siku zote yamekuwa wazi kwa kila mmoja. Mungu hajawahi kuficha kimakusudi kiini Chake, tabia Yake au mapenzi Yake. Ni vile tu mwanadamu hajali kuhusu kile ambacho Mungu anafanya, mapenzi Yake ni yapi—ndio maana uelewa wa binadamu kumhusu Mungu ni finyu mno. Kwa maneno mengine, wakati Mungu anaficha nafsi Yake, Yeye pia Anasimama kando ya mwanadamu kila wakati, akionyesha waziwazi mapenzi Yake, tabia Yake na kiini chake halisi siku zote. Kimsingi, nafsi ya Mungu pia iko wazi kwa watu lakini kutokana na upofu na kutotii kwa binadamu, siku zote hawawezi kuuona kuonekana kwa Mungu. Hivyo kama hali iko hivyo, basi si kuelewa tabia ya Mungu na Mungu Mwenyewe kuna faa kuwa rahisi mno kwa kila mmoja? Hili ni swali gumu sana kujibu, sivyo? Mnaweza kusema ni rahisi, lakini wakati watu wengine wanatafuta kumjua Mungu, hatimaye hawamjui Yeye au kupata uelewa wa wazi kumhusu Yeye—siku zote ni jambo lililojaa ukungu na lisiloleweka. Lakini mkisema si rahisi, hilo si sahihi vilevile. Baada ya kuwa mlengwa wa kazi ya Mungu kwa muda mrefu, kila mmoja anafaa, kupitia uzoefu wake, kuwa amepitia kwa kweli mambo mbalimbali na Mungu. Anafaa kuwa amehisi Mungu angalau kwa kiwango fulani katika moyo wake au awe amekuwa na mawasiliano ya kiroho na Mungu, na anafaa angalau kuwa alikuwa na ufahamu kiasi tambuzi kuhusu tabia ya Mungu au kupata uelewa fulani kumhusu Yeye. Kuanzia wakati binadamu alianza kumfuata Mungu hadi sasa, mwanadamu amepokea mengi mno, lakini kutokana na sababu za aina zote—uhodari wa kimasikini ya kibinadamu, kutojua, uasi, na nia mbalimbali—wanadamu wamepoteza mambo mengi mno. Je, Mungu hajampatia mwanadamu mali ya kutosha? Ingawaje Mungu huficha nafsi Yake kutoka kwa wanadamu, Anawatosheleza mahitaji yao kwa kile Anacho na alichio, na hata maisha Yake; maarifa ya binadamu ya Mungu hayafai kuwa vile yalivyo tu sasa. Ndiyo maana Nafikiri inahitajika kuwa na ushirika zaidi na nyinyi kuhusu mada ya kazi ya Mungu, kuhusu tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe. Kusudio ni ili miaka elfu ya utunzaji na fikira ambayo Mungu amemwagia binadamu isije ikaisha bure bilashi, na ili mwanadamu aweze kuelewa kwa dhati na kutambua mapenzi ya Mungu kwake. Ni ili watu waweze kusonga mbele kwenye hatua mpya ya maarifa yao kumhusu Mungu. Itaweza pia

kumrudisha Mungu katika nafasi Yake inayofaa kwenye mioyo ya watu yaani kumfanyia Yeye haki.

Ili kuelewa tabia ya Mungu na Mungu Mwenyewe lazima muanzie na jambo dogo sana. Jambo hilo dogo sana mnalopaswa kuanzia ni nini? Kwanza kabisa, Nimezikusanya baadhi ya sura kutoka kwenye Biblia. Taarifa iliyo hapa chini inayo mistari ya Biblia, ambayo yote inahusiana na mada ya tabia ya Mungu, kazi ya Mungu na Mungu Mwenyewe. Nilipata dondoo hizi mahususi kama nyenzo za marejeleo ili kuwasaidia kujua kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe. Hapa Nitayashiriki nanyi ili muweze kuona ni aina gani ya tabia na kiini cha Mungu ambacho kimefichuliwa kupitia kwa kazi Yake ya kitambo lakini watu hawajui kukihusu. Sura hizi zinaweza kuwa nzee, lakini mada tunayowasiliana ni kitu kipya ambacho watu hawana na hawajawahi kusikia. Baadhi yenu huenda mkapata hazieleweki—je, kule kuwataja Adamu na Hawa na kurudi kwa Nuhu si kurudia hatua sawa tena? Haijalishi ni nini mnafikiria, sura hizi ni zenye manufaa kwa mawasiliano ya mada hii na zinaweza kutumika kama maandishi ya mafunzo au nyenzo za matumizi ya kwanza katika ushirika wa leo. Mtaelewa nia Zangu za kuchagua sehemu hizi kufikia wakati Nitakapoumaliza ushirika huu. Wale ambao wamesoma Biblia awali huenda wameona mistari hii michache lakini huenda hawajaelewa. Hebu tuangalie haraka kwanza kabla ya kupitia mistari hii mmoja baada ya mwingine kwa kina zaidi.

Adamu na Hawa ni mababu wa mwanadamu. Kama itabidi tutaje wahusika kutoka kwenye Biblia, basi lazima tuanzie na wawili hawa. Kisha Nuhu, mababu wa pili wa mwanadamu. Mhusika wa tatu ni nani? (Ibrahimu.) Je, nyote mnajua hadithi ya Ibrahimu? Baadhi yenu mnaweza kujua, lakini kwa baadhi yenu huenda isiwe wazi sana. Nani ndiye mhusika wa nne? Ni nani anayetajwa kwenye hadithi ya kuangamizwa kwa Sodom? (Lutu.) Lakini Lutu hajarejelewa hapa. Ni nani anayerejelewa? (Ibrahimu.) Kitu kikuu kilichotajwa kwenye hadithi ya Ibrahimu ni kile Yehova Mungu alikuwa amesema. Je mnaona haya? Nani ndiye mhusika wa tano? (Ayubu.) Je, Mungu hataji mengi kwenye hadithi ya Ayubu wakati wa awamu hii ya kazi Yake? Basi mnajali sana kuhusu hadithi hii? Kama mnajali sana, je mmeisoma hadithi ya Ayubu kwenye Biblia kwa umakinifu? Je, mnajua ni mambo gani Ayubu alisema, ni mambo gani aliyofanya? Wale ambao wameisoma hadithi hiyo sana, ni mara ngapi mmeisoma? Je, mnaisoma mara kwa mara? Akina dada kutoka Hong Kong, tafadhali tuambieni. (Mimi niliisoma mara kadhaa hapo awali tulipokuwa katika Enzi ya Neema.) Hamjawahi soma tena tangu hapo? Kama ni hivyo, basi hiyo ni aibu kubwa. Wacha Niwaambie: Katika awamu hii ya kazi ya Mungu Alimtaja Ayubu mara nyingi, na hilo ni onyesho la nia Zake. Kwamba Alimtaja Ayubu mara nyingi lakini umakini wenu haukuzinduliwa ni thibitisho kwa ukweli kwamba: Hamna haja ya kuwa watu ambao ni wazuri na watu wanaomcha Mungu na kujiepusha na maovu. Hii ni kwa sababu mnatosheka tu na kuwa na wazo la juujuu kuhusu hadithi ya Ayubu iliotajwa na Mungu.

Mnatosheka na uelewa wa juujuu wa hadithi yenyewe, lakini hamjali kuhusu na hamtaki kufahamu maelezo ya Ayubu ni nani na kusudio linalomfanya Mungu kumrejelea Ayubu mara kadhaa. Kama hata hamjali mtu kama huyo ambaye Mungu amesifu, basi ni nini hasa mnayotilia maanani? Kama hamjali kuhusu na hamjaribu kuelewa mhusika muhimu sana kama huyu ambaye Mungu amemtaja, basi hiyo inasema nini kuhusu mwelekeo wenu katika neno la Mungu? Hilo si jambo baya? Je, hiyo haithibitishi kwamba wengi wenu hawajihusishi katika mambo ya kimatendo na nyinyi nyote hamfuatili ukweli? Kama unafuatilia ukweli, utatilia maanani kwa lazima watu ambao Mungu ameidhinisha na hadithi za wahusika ambazo Mungu amezungumzia. Haijalishi kama unaweza kutenda yanavyohitaji au kuona kuwa hadithi zake ni dhahiri shahiri, utaenda haraka na kuisoma, kujaribu kuifahamu, kupata njia za kufuata mfano wake, na kufanya kile unachoweza kwa uwezo wako bora zaidi. Hiyo ndiyo tabia ya mtu anayetamani ukweli. Lakini ukweli ni kwamba wengi wenu mlioketi hapa hamjawahi kuisoma hadithi ya Ayubu. Hii kwa kweli inaniambia kitu.

Hebu turudi katika mada niliyokuwa Nikizungumzia muda mfupi uliopita. Sehemu hii ya maandiko inayoshughulikia Enzi ya Sheria ya Agano la Kale ni haswa hadithi za wahusika Nilizokuwa nimedondoa. Hizi ni hadithi zilizoeleweka kwa watu wengi ambao wamesoma Biblia. Wahusika hawa ni wawakilishi sana. Wale waliosoma hadithi hizi wataweza kuhisi kwamba kazi ambayo Mungu amewafanyia wao na maneno ambayo Mungu amewazungumzia yanashikika na yanafikika kwa watu wa leo. Unaposoma hadithi hizi na rekodi hizi kutoka kwenye Biblia, utaweza kuelewa namna ambavyo Mungu alivyofanya kazi Yake na namna alivyoshughulikia watu wakati huo. Lakini kusudio la Mimi kutafuta sura hizi leo si eti kwamba uweze kujaribu kung'amua hadithi hizi na wahusika ndani zao. Badala yake, ni ili uweze kupitia kwa hadithi za wahusika hawa, kuona vitendo vya Mungu na tabia Yake, na hivyo kurahisisha kujua na kuelewa Mungu, kuuona upande halisi Wake yeye, kusitisha kufikiria kwako, na kukomesha dhana zako kuhusu Yeye, na kusitisha imani yako na kuitoa katika hali ya kutokuwa na hakika. Kujaribu kuifahamu tabia ya Mungu na kuielewa na kupata kujua Mungu mwenyewe bila ya msingi, kunaweza mara nyingi kukufanya kuhisi kama mtu asiyeweza, asiye na nguvu, na asiye na hakika ni wapi wataanzia. Na ndiyo maana Nilifikiria ni wazo zuri kutumia mbinu kama hii na mtazamo ili kukufanya kumwelewa Mungu kwa njia bora zaidi, na kwa uhalisia zaidi kutambua na kushukuru mapenzi ya Mungu na kupata kujua tabia ya Mungu na Mungu Mwenyewe na kukufanya kuhisi kwa dhati uwepo wa Mungu na kushukuru mapenzi Yake kwa wanadamu. Je, haya si ya manufaa kwenu? Sasa mnahisi vipi ndani ya mioyo yenu mnapoziangalia hadithi hizi na maandiko haya tena? Je, mnafikiria maandiko haya Niliyoyachukua yamezidi kuliko kawaida? Lazima Nitilie mkazo tena kile Nimetoka tu kuwaambia. Nia ya kuwaruhusu kusoma hadithi hizi za wahusika ni kuwasaidia kuelewa namna

ambavyo Mungu anafanya kazi Yake kwa watu na mwelekeo Wake kwa wanadamu. Ni kupitia nini ndipo mtaweza kuelewa haya? Kupitia kwa kazi ambayo Mungu amefanya kitambo, na kuunganisha pamoja na kazi ambayo Mungu anafanya sasa hivi kuwasaidia kuelewa mambo mbalimbali kuhusu Yeye. Mambo haya mbalimbali ni ya kweli, na lazima yajulikane na yatambulike na wote wanaotaka kumjua Mungu.

Tutaanza sasa na hadithi ya Adamu na Hawa. Kwanza, hebu tuyasome maandiko.

1. Adamu na Hawa

1) Amri ya Mungu kwa Adamu

Mwa 2:15-17 Naye Yehova Mungu akamchukua mtu huyo, na kumweka ndani ya bustani ya Eden ili ailime na kuihifadhi. Yehova Mungu akamwamrisha mtu huyo, akisema, Unaweza kula kwa uhuru matunda kutoka miti yote ya bustani: Lakini kutoka mti wa maarifa ya mema na maovu, usiyale: kwa kuwa katika siku ambapo utakula matunda kutoka mti huo bila shaka utakufa.

Je, mlielewa chochote kutoka kwenye mistari hii? Je, ni vipi ambavyo sehemu hii ya maandiko inavyo wafanya kuhisi? Kwa nini “Amri ya Mungu kwa Adamu” ilidondolewa kutoka kwa maandiko? Je, kila mmoja wenu sasa anayo picha ya Mungu na Adamu katika akili yenu? Mnaweza kujaribu kufikiria: Kama ni nyinyi mliokuwa katika tukio hilo, je, Mungu katika moyo wenu angekuwa vipi? Ni hisia gani ambazo picha hii zinafanya mhisi? Hii ni picha ya kusesimua na ya kutuliza moyo. Ingawaje kunaye Mungu tu na binadamu ndani yake, ule ukaribu kati yao unastahili kuonewa wivu: Upendo mwingi wa Mungu amepewa binadamu kwa ukarimu, unamzunguka binadamu; binadamu ni mnyofu na asiye na hatia, aliye huru kabisa na asiyejali chochote, anayeishi kwa furaha kwa uangalizi wa jicho la Mungu; Mungu anaonyesha hali ya kujali binadamu huku naye binadamu anaishi katika ulinzi na baraka za Mungu; kila kitu binadamu anachofanya na kusema kinaunganishwa kwa karibu na Mungu na hakiwezi kutofautishwa.

Mnaweza kusema kwamba hii ndiyo amri ya kwanza ya Mungu aliyotoa kwa binadamu tangu kumuumba yeye. Je, amri hii ina nini? Amri hii inayo mapenzi ya Mungu, lakini pia inayo wasiwasi Wake kwa wanadamu. Hii ndiyo amri ya kwanza ya Mungu na pia ndio mara ya kwanza Mungu anakuwa na wasiwasi kuhusu binadamu. Hivi ni kusema, Mungu analo jukumu kwa binadamu tangu ule wakati alipomuumba yeye. Jukumu Lake ni lipi? Lazima amlinde binadamu, kumwalia binadamu. Anatumai kwamba binadamu anaweza kuamini na kutii maneno Yake. Hili pia ndilo tarajio la kwanza la Mungu kwa binadamu. Na ni kwa tarajio hili kwamba Mungu anasema yafuatayo: “Unaweza kula kwa uhuru matunda kutoka miti yote ya

bustani: Lakini kutoka mti wa maarifa ya mema na maovu, usiyale: kwa kuwa katika siku ambapo utakula matunda kutoka mti huo bila shaka utakufa.” Maneno haya rahisi yanawakilisha mapenzi ya Mungu. Yanafichua pia kwamba moyo wa Mungu tayari umeanza kuonyesha hali ya kujali binadamu. Miongoni mwa mambo yote, ni Adamu pekee aliyeumbwa kwa taswira ya Mungu; Adamu alikuwa kiumbe wa pekee aliye hai aliye na pumzi ya uhai ya Mungu; angeweza kutembea na Mungu, kuzungumza na Mungu. Na ndiyo maana Mungu alimpa amri kama hiyo. Mungu aliweka wazi katika amri hii kile binadamu anaweza kufanya, na vilevile akaweza wazi kile asichoweza kufanya.

Katika maneno haya machache rahisi, tunauona moyo wa Mungu. Lakini ni aina gani ya moyo tunaouona? Je, kuna upendo katika moyo wa Mungu? Je, upendo huo unao hali yoyote ya kujali ndani yake? Upendo wa Mungu na kujali kwake katika mistari hii hakuwezi kutambulika na kuthaminiwa tu na watu, lakini unaweza pia kuhisiwa vizuri na kwa kweli. Hayo ni kweli? Kwa vile nimesema tayari mambo haya, bado mnafikiria kwamba haya ni maneno machache tu rahisi? Si rahisi hivyo, kweli? Mngeweza kuona hivi awali? Kama Mungu mwenyewe angekuambia maneno haya machache mngehisi vipi ndani yenu? Kama wewe si mtu mwenye utu, kama moyo wako ni baridi kama barafu, basi usingehisi chochote, usingethamini upendo wa Mungu, na usingejaribu kuuelewa moyo wa Mungu. Lakini kama wewe ni mtu mwenye dhamiri, mwenye ubinadamu, basi utahisi tofauti. Utahisi joto, utahisi kuwa umetunzwa na umependwa, na utahisi furaha. Je, hayo ni kweli? Unapohisi mambo haya, utatenda vipi kwa Mungu? Utahisi ukiwa umeunganishwa kwa Mungu? Utampenda na kumheshimu Mungu kutoka kwenye sakafu ya moyo wako? Moyo wako utakuwa karibu zaidi na Mungu? Unaweza kuona kutoka kwa haya namna ambavyo upendo wa Mungu ulivyo muhimu kwa binadamu. Lakini kile kilicho muhimu zaidi ni kuthamini na kufahamu kwa binadamu upendo huu wa Mungu. Kwa hakika, Mungu hasemi mambo mengi yanayofanana kwenye awamu hii ya kazi Yake? Lakini je, watu wa leo wanauthamini moyo wa Mungu? Je, mnaweza kung’amua mapenzi ya Mungu Niliyoyazungumzia muda mfupi uliopita? Hamwezi hata kutambua mapenzi ya Mungu wakati yanaonekana waziwazi, yanaweza kushikika na ni halisi. Na ndiyo maana Nasema hamna maarifa na uelewa halisi wa Mungu. Je, haya si kweli? Hayo tu ndiyo yote tutakayowasiliana nanyi kwenye sehemu hii.

2) Mungu Amuumba Hawa

Mwa 2:18-20 Yehova Mungu akasema, Si vizuri kuwa mtu huyo akuwe peke yake; nitamuambia msaidizi anayefanana na yeye. Na kutoka kwa ardhi Yehova Mungu akaumba wanyama wote wa msituni, na ndege wote wa angani; na akawaletea kwa Adamu ndiyo aone majina ambayo angewapa: na chochote ambacho Adamu alikiita kiumbe hai, hilo ndilo likawa

jina lake kuanzia hapo. Naye Adamu akawapa wanyama wote wa kufugwa majina, na ndege wa hewani, na wanyama wote wa mwituni; lakini kwa Adamu hakupatikana msaidizi ambaye alifanana na yeye.

Mwa 2:22-23 Nao ubavu, ambao Yehova Mungu aliuchukua kutoka kwa Adamu, Yeye akaufanya uwe mwanamke, na akampeleka kwa Adamu. Naye Adamu akasema, Huyu sasa ni mfupa wa mifupa yangu, na nyama ya nyama zangu: ataitwa Mwanamke, kwa kuwa amechukuliwa kutoka kwa Mwanamume.

Kuna msitari mmoja muhimu kwenye sehemu hii ya Maandiko: “chochote ambacho Adamu alikiita kiumbe hai, hilo ndilo likawa jina lake kuanzia hapo.” Kwa hivyo ni nani aliyepatia viumbe wote haya majina yao? Alikuwa Adamu, si Mungu. Msitari huu unamwambia mwanadamu ukweli: Mungu alimpa binadamu werevu alipomuumba Yeye. Hivi ni kusema kwamba, werevu wa binadamu ulitoka kwa Mungu. Hili ni kweli. Lakini kwa nini? Baada ya Mungu kumuumba Adamu, Adamu alienda shuleni? Je, alijua namna ya kusoma? Baada ya Mungu kuwaumba viumbe hai mbalimbali, je, Adamu aliwatambua viumbe hawa wote? Je, Mungu alimwambia majina ya viumbe hao? Bila shaka, Mungu pia hakumfunza namna ya kutunga yale majina ya viumbe hawa. Huo ndio ukweli! Basi alijua vipi namna ya kupatia viumbe hawa hai majina yao na aina gani ya majina ya kuwapatia? Haya yote yanahusiana na swali kuhusu ni nini ambacho Mungu aliongezea kwa Adamu alipomuumba yeye. Ukweli unathibitisha kwamba wakati Mungu alipomuumba binadamu Alikuwa ameongezea werevu kwake. Huu ni ukweli muhimu sana. Je, nyinyi nyote mmesikiliza kwa makini? Kunao ukweli mwingine muhimu ambao unafaa kuwa wazi kwenu? Baada ya Adamu kuwapatia viumbe hai majina yao, majina haya yalipangwa kwenye msamiati wa Mungu. Kwa nini Ninasema hivyo? Hii pia inahusisha tabia ya Mungu, na lazima Niielezee.

Mungu alimuumba binadamu, Akapumua maisha ndani yake, na pia Akampa baadhi ya werevu Wake, uwezo Wake, na kile Anacho na alichu. Baada ya Mungu kumpa binadamu mambo haya yote, binadamu aliweza kufanya baadhi ya mambo haya kwa uhuru na kufikiria pekee yake. Kama kile binadamu anaunda na kufanya ni kizuri machoni mwa Mungu, basi Mungu anakikubali na haingilii kati. Kama kile binadamu anafanya ni sahihi, basi Mungu atakiacha tu kiwe hivyo milele. Kwa hivyo kauli hii “chochote ambacho Adamu alikiita kiumbe hai, hilo ndilo likawa jina lake kuanzia hapo” inaonyesha nini? Inaopendekeza kwamba Mungu hakufanya marekebisho yoyote kwa majina ya wale viumbe mbalimbali hai. Jina lolote lile ambalo Adamu alimwita, Mungu alisema “Ndiyo” na akasajili jina hilo hivyo. Je, Mungu alionyesha maoni yoyote? La, hilo ni hakika. Kwa hivyo, mnaona nini hapa? Mungu Alimpa binadamu werevu naye binadamu akautumia werevu wake aliopewa na Mungu kufanya mambo.

Kama kile binadamu anafanya ni kizuri machoni mwa Mungu, basi kinathibitishwa, kutambulika, na kukubalika na Mungu bila ya utathmini au upinzani wowote. Hili ni jambo ambalo hakuna mtu wala roho wa maovu, wala Shetani, anaweza kufanya. Je, mnauona ufunuo wa tabia ya Mungu hapa. Je, mwanadamu, mwanadamu aliyepotoshwa, au Shetani anaweza kuwakubali wengine kuwawakilisha katika kufanya mambo huku wakitazama? Bila shaka la! Je, wanaweza kupigania cheo na yule mtu mwingine au nguvu nyingine ambayo ni tofauti na wao? Bila shaka wangepanya hivyo! Na kwa muda huo, kama angekuwa ni mtu aliyepotoshwa au Shetani aliyekuwa na Adamu, bila shaka wangepataa kile ambacho Adamu alikuwa akifanya. Ili kuthibitisha kwamba wanao uwezo wa kufikiria kwa uhuru na wanayo maono yao binafsi na ya kipekee, wangepataa kabisa kila kitu alichofanya Adamu: “Unataka kukiita hivyo? Kwa kweli, sitakiita hivyo, nitakiita hivi; ulikiita Tom lakini mimi nitakiita Harry. Lazima nionyeshe ustadi wangu.” Haya ni aina gani ya asili? Hii ni asili ya kiburi kisicho na mipaka? Lakini Mungu anayo tabia kama hii? Je, Mungu alikuwa na upinzani wowote usiokuwa wa kawaida kwa mambo haya ambayo Adamu alifanya? Jibu ni bila shaka la! Kati ya tabia ambayo Mungu anafichua, hakuna hata chembe ya ubishi, ya kiburi, au kujigamba kwa nafsi. Hilo liko wazi kabisa hapa. Hili ni jambo dogo tu, lakini kama huelewi kiini cha Mungu, kama moyo wako hautajaribu kujua namna ambavyo Mungu anatenda na mwelekeo wa Mungu ni ipi, basi hutajua tabia ya Mungu au kuyaona maonyesho na ufunuo wa tabia ya Mungu. Je, hayo si kweli? Je, unakubali kile Nimetoka tu kukuelezea? Kwa kujibu matendo ya Adamu, Mungu hakutangaza kwa sauti kwamba, “Umefanya vyema. Umefanya sahihi Ninakubali.” Katika Moyo Wake, hata hivyo, Mungu aliidhinisha, akathamini, akashangilia kile Adamu alikuwa amefanya. Hili ndilo jambo la kwanza tangu uumbaji ambalo binadamu alikuwa amemfanyia Mungu akifuata maagizo Yake. Ni jambo ambalo binadamu alifanya badala ya Mungu na kwa niaba ya Mungu. Mbele ya macho yake, hili lilitokana na werevu Aliokuwa amempa binadamu. Mungu aliliona kama jambo zuri, kitu kizuri. Kile ambacho Adamu alifanya wakati huo kilikuwa maonyesho ya kwanza ya werevu wa Mungu kwa binadamu. Hili lilikuwa onyesho zuri kutoka kwa maoni ya Mungu. Kile Ninachotaka kuwaambia nyinyi hapa ni kwamba nia ya Mungu katika kuongezea sehemu ya kile Anacho na alichu na werevu wake kwa binadamu ilikuwa ili mwanadamu aweze kuwa kiumbe hai anayemwonyesha Yeye. Kwa kiumbe hai kama huyo kufanya mambo hayo kwa niaba yake, ilikuwa ndicho hasa kile Mungu alikuwa akitamani kuona.

3) Mungu Awatengenezea Adamu na Hawa Nguo za Ngozi

Mwa 3:20-21 Adamu akampa mke wake jina la Hawa; kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa mama ya wote wenye uhai. Pia Yehova Mungu akawatengenezea Adamu na mke wake nguo za ngozi; na akawavisha.

Hebu tuangalie kifungu hiki cha tatu, kinachosema kwamba, kunayo maana katika jina Adamu alimpa Hawa, kweli? Hii inaonyesha kwamba baada ya kuumbwa, Adamu alikuwa na fikira zake na alielewa mambo mengi. Lakini kwa sasa, hatutasoma na kuchunguza kile alichoelewa au kwa kiwango kipi alielewa kwa sababu hiyo si hoja kuu Ninayotaka kuzungumzia kwenye kifungu hiki cha tatu. Hivyo hoja kuu katika kifungu cha tatu ni gani? Hebu na tuangalie mstari huo, “Pia Yehova Mungu akawatengenezea Adamu na mke wake nguo za ngozi; na akawavisha.” Kama hatutakuwa na ushirika kuhusu mstari huu wa maandiko leo, huenda hamtawahi kutambua uzito ulio katika maneno haya. Kwanza, hebu niwape vidokezo fulani. Panua kufikiria kwenu na kuona picha ya bustani ya Edeni, huku Adamu na Hawa wakiishi ndani. Mungu anaenda kuwatembelea lakini wanajificha kwa sababu wako uchi. Mungu hawezi kuwaona, na baada ya kuwaita wao, wanasema, “Hatuwezi kuthubutu kukuona kwa sababu tuko uchi.” Hawathubutu kumwona Mungu kwa sababu wako uchi. Kwa hivyo Yehova Mungu anawafanya nini? Maandishi asilia yanasema: “Pia Yehova Mungu akawatengenezea Adamu na mke wake nguo za ngozi; na akawavisha.” Sasa mnajua kile Mungu alitumia kutengeneza nguo zao? Mungu alitumia ngozi za wanyama kutengeneza nguo zao. Hivyo ni kusema, nguo ambazo Mungu alitengenezea binadamu zilikuwa za koti la manyoya. Hiki ndicho kilichokuwa kipande cha kwanza cha nguo ambacho Mungu alitengenezea binadamu. Koti la manyoya ni mavazi ya soko la vitu vya bei ghali kwa viwango vya leo, kitu ambacho si kila mtu anaweza kumudu kuvaa. Kama mtu atakuuliza: Kipande cha kwanza cha nguo kilichovaliwa na wazee wa wanadamu kilikuwa kipi? Unaweza kujibu: Kilikuwa ni koti la manyoya. Nani aliyetengeneza hilo koti la manyoya? Unaweza kujibu zaidi: Mungu alilitengeneza! Hiyo ndiyo hoja kuu: Nguo hii ilitengenezwa na Mungu. Je, hilo ni jambo la kutilia maanani, sivyo? Kwa vile sasa nimetoka kukifafanua, picha imeibuka katika akili zenu? Kunafaa kuwa angaa na mpangilio wa juu kukihusu. Hoja ya kuwaambia haya leo si kuwafahamisha kuhusu kipande cha kwanza cha nguo cha binadamu kilikuwa nini. Hivyo hoja ni gani? Hoja si lile koti la manyoya, lakini namna ya kujua tabia na uwepo na nafsi zilizofichuliwa na Mungu alipokuwa Akifanya hivi.

“Pia Yehova Mungu akawatengenezea Adamu na mke wake nguo za ngozi; na akawavisha,” Katika tukio hili, ni wajibu gani ambao tunamwona Mungu akiuchukua Anapokuwa na Adamu na Hawa? Na ni katika aina gani ya uajibu ambao Mungu anajitokeza katika ulimwengu akiwa tu na wanadamu wawili? Kutekeleza wajibu wa Mungu? Kaka na dada kutoka Hong Kong, tafadhali jibuni. (Kutekeleza wajibu wa mzazi.) Kaka na dada kutoka Korea Kusini, ni wajibu wa aina gani mnafikiria Mungu anatekeleza hapa? (Kiongozi wa familia.) Kaka na dada kutoka Taiwan, mnafikiria nini? (Wajibu wa mtu katika familia ya Adamu na Hawa, wajibu wa mwanafamilia.) Baadhi yenu mnafikiria kuwa Mungu anajitokeza kama

mwanafamilia wa Adamu na Hawa, huku baadhi wakisema kwamba Mungu anajitokeza kama kiongozi wa familia na wengine wanasema kwamba Anajitokeza kama mzazi. Haya yote yanafaa sana. Lakini ni nini hasa Ninachotilia mkazo hapa? Mungu aliwaumba watu hawa wawili na kuwashughulikia kama mtu na mwandani Wake. Akiwa ndiye mwanafamilia pekee wao, Mungu aliangalia kuishi kwao na pia akakidhi mahitaji yao ya kimsingi. Hapa, Mungu anajitokeza kama mzazi wa Adamu na Hawa. Huku Mungu akifanya haya, binadamu haoni namna ambavyo Mungu alivyo mkuu; haoni mamlaka ya juu zaidi ya Mungu, hali Yake ya mafumbo, na hasa haoni hasira au adhama Yake. Kile anachoona tu ni unyenyekevu wa Mungu, upendo Wake, kujali Kwake binadamu na jukumu Lake na utunzaji Wake kwake yeye. Mwelekeo na njia ambayo Mungu alishughulikia Adamu na Hawa ni sawa na namna ambavyo wazazi wa kibinadamu wanavyoonyesha hali ya kuwajali watoto wao binafsi. Ni kama pia namna ambavyo wazazi wa kibinadamu wanavyopenda, kuangalia, na kutunza watoto wao binafsi wa kiume na kike—halisia, namna ya kuonekana, na kushikika. Badala ya kujiweka Yeye Mwenyewe katika cheo cha juu na cha utukufu, Mungu mwenyewe alitumia ngozi kutengeneza nguo za binadamu. Haijalishi kama koti hili la manyoya lilitumika kufunika uchi wao au wao kujikinga dhidi ya baridi. Kwa ufupi, nguo hii iliyotumika kuufunika mwili wa binadamu ilitengenezwa na Mungu mwenyewe kwa mikono Yake mwenyewe. Badala ya kuitengeneza tu kupitia kwa fikira au kwa mbinu za kimiujiza kama watu wanavyofikiria, Mungu alikuwa amefanya kitu cha halali kwa binadamu ambacho binadamu anafikiria Mungu hawezi na hafai kufanya. Kitu hiki kinaweza kuwa rahisi ambacho baadhi huenda hata wasifikirie kwamba kinastahili kutajwa, lakini kinawaruhusu pia wale wote wanaomfuata Mungu lakini awali walikuwa na mawazo yasiyoeleweka kuhusu Yeye kuweza kupata maono kuhusu ukweli na uzuri Wake, na kuuona uaminifu Wake na asili Yake ya unyenyekevu. Kinawafanya watu wenye kiburi kisicho na kifani wanaofikiria kwamba wako juu na wanao utukufu kuinamisha vichwa vyao kwa aibu mbele ya ukweli na unyenyekevu wa Mungu. Hapa, ukweli na unyenyekevu wa Mungu unawezesha zaidi watu kuona namna ambavyo Anapendeka. Kwa kinyume cha mambo, yule Mungu mkubwa sana, Mungu anayependeka na yule Mwenyezi Mungu katika mioyo ya watu ni mdogo sana, asiyevutia, na asiyeweza kuhimiliwa hata mara moja. Unapouona mstari huu na kuisikia hadithi hii, unamkasirikia Mungu kwa sababu Alifanya kitu kama hiki? Baadhi ya watu wanaweza kufanya hivyo, lakini kwa wengine itakuwa ni tofauti kabisa. Watafikiri Mungu ni mkweli na anapendeka, na hasa ni ule ukweli na uzuri wa Mungu ndiyo unaowafurahisha. Kwa kadri wanavyoona ule upande wa kweli wa Mungu, ndipo wanapothamini uwepo wa kweli wa upendo wa Mungu, umuhimu wa Mungu katika mioyo yao, na namna anavyosimama kando yao kila muda.

Kwa wakati huu, tunafaa kuunganisha mazungumzo yetu na sasa. Kama Mungu angeweza

kufanya mambo haya madogo mbalimbali kwa binadamu Aliowaumba hapo mwanzo kabisa, hata vitu vingine ambavyo watu hawangethubutu kufikiria ama kutarajia, basi naye Mungu angewafanyia watu leo mambo kama hayo? Baadhi ya watu husema, “Ndiyo!” Kwa nini hivyo? Kwa sababu kiini cha Mungu si bandia, uzuri Wake si bandia. Kwa sababu kiini cha Mungu kwa kweli kipo, na si kitu kilichoongezewa tu na wengine na bila shaka si kitu ambacho kinabadilika na mabadiliko ya muda, mahali, na enzi. Ukweli na uzuri wa Mungu unaweza kwa kweli kuonyeshwa kupitia kufanya jambo ambalo watu wanafikiria si la kipekee na ni dogo, jambo ambalo ni dogo sana kiasi cha kwamba watu hata hawafikirii angeweza kufanya. Mungu si mnaifi. Hakuna kupiga chuku, kufunika ukweli, majivuno au kiburi katika tabia na kiini Chake. Siku zote Hajigambi, lakini badala yake Anapenda, Anaonyesha hali ya kujali, Anaangalia, na kuwaongoza wanadamu Aliowaumba kwa uaminifu na dhati. Haijalishi ni kiwango kipi ambacho watu wanaweza kuthamini, kuhisi, au kuona, Mungu kwa hakika anafanya mambo haya. Je, kujua kwamba Mungu anacho kiini kama hicho kunaweza kuathiri upendo wa watu kwake Yeye? Kutaweza kushawishi namna wanavyomcha Mungu? Ninatumai utakapoelewa upande halisi wa Mungu utaweza kuwa hata karibu zaidi na Yeye na kuweza kuthamini hata zaidi na kwa kweli upendo Wake na utunzaji Wake kwa wanadamu, huku wakati huohuo pia kumpa moyo wako na kutowahi tena kuwa na shaka au wasiwasi wowote kwake Yeye. Mungu anafanya kimyakimya kila kitu kwa ajili ya binadamu, akifanya kimyakimya kupitia ukweli, uaminifu, na upendo Wake. Lakini siku zote Hana hofu au majuto yoyote kwa yale yote Anayofanya, wala hahitaji mtu yeyote kumlipa Yeye kwa njia yoyote au kuwa na nia za kuwahi kupokea kitu kutoka kwa wanadamu. Kusudio tu la kila kitu Alichowahi kufanya ni ili Aweze kupokea imani na upendo wa kweli kutoka kwa wanadamu. Hebu tuhitimishe mada hii ya kwanza hapa.

Je, mazungumzo haya yamewasaidia? Yamewasaidia kwa kiasi kipi? (Uelewa na maarifa zaidi kuhusu upendo wa Mungu.) (Mbinu hii ya mawasiliano inaweza kutusaidia katika siku za mbele ili kuweza kuthamini zaidi neno la Mungu, kufahamu hisia alizokuwa nazo na maana ya mambo Aliyoyasema Alipoyasema, na kuhisi namna Alivyohisi wakati huo.) Je, yupo yeyote kati yenu anayehisi hata zaidi uwepo halisi wa Mungu baada ya kuyasoma maneno haya? Je, mnahisi uwepo wa Mungu si mtupu wala wa kutiliwa mashaka tena? Pindi mnapokuwa na hisia hii, mnahisi kwamba Mungu yupo tu kando yenu? Pengine hisia hiyo si ya dhahiri kwa sasa hivi au hamtaweza kuihisi sasa hivi bado. Lakini siku moja, mtakapokuwa na shukrani ya kina na ya kweli na maarifa halisi kuhusu tabia na kiini cha Mungu ndani ya moyo wako, utahisi kwamba Mungu yupo tu kando yako—ni vile tu kwamba haujawahi kumkubali kwa kweli Mungu ndani ya moyo wako. Haya ni halisi.

Mnafikiria vipi kuhusu mbinu hii ya mawasiliano? Mnaweza kuiendeleza? Mnafikiria aina

hii ya ushirika kuhusu mada ya kazi ya Mungu na tabia ya Mungu ni nzito? Mnahisi vipi? (Vizuri sana, kuchangamka.) Ni nini kilichowafanya kuhisi vizuri? Kwa nini mlichangamka? (Ilikuwa sawa na kurudi kwenye Bustani ya Edeni, kurudi kuwa kando ya Mungu.) “Tabia ya Mungu” kwa kweli ni mada ambayo haijaoeleka sana na kila mmoja, kwa sababu kile ambacho unafikiria kwa kawaida, kile unachosoma kwenye vitabu au kusikia kwenye ushirika, siku zote hukufanya kuhisi kama mtu asiyeona akimgusa ndovu—unahisi tu kila pahali kwa kutumia mikono yako, lakini kwa hakika huoni chochote kwa macho yako. “Mguso wa mkono” hauwezi tu kukupa mpangilio wa kimsingi wa maarifa ya Mungu, wacha hata dhana iliyo wazi. Kile ambacho mguso wa mkono unakupatia ni kufikiria zaidi, kiasi kwamba huwezi kufafanua kwa uhakika tabia ya Mungu na kiini halisi. Badala yake, masuala haya ya kutokuwa na uhakika yanayotokana na kufikiria kwako huwa siku zote yanaonekana kujaza moyo wako na shaka. Wakati ambapo huwezi kuwa na uhakika kuhusu kitu na ilhali bado unajaribu kukielewa, ndani ya moyo wako bado siku zote kutaendelea kuwa na mambo yanayopingana na kukinzana, na wakati mwingine huenda hata yakabadilika na kuwa shida, na kukufanya kuhisi ni kana kwamba umepoteza kitu. Je, si jambo la kusikitisha sana unapotaka kumtafuta Mungu, kumjua Mungu, na kumwona Yeye waziwazi, lakini siku zote kutoweza kupata majibu? Bila shaka, maneno haya yanalengwa kwa wale wanaotamani kutafuta uwezo wa kumuheshimu sana Mungu na kuridhisha Mungu. Kwa wale watu ambao hawatilii maanani mambo kama haya, hili kwa hakika si muhimu kwa sababu wanatumaini kwamba ni bora zaidi kuwa uhalisi na uwepo wa Mungu uwe ni ngano ya kale au ndoto, ili waweze kufanya chochote wanachotaka, ili waweze kuwa wale wakubwa zaidi na wenye umuhimu zaidi, na kuweza kutenda vitendo vya maovu bila ya kujali athari zake, na hivyo basi kutoweza kukabiliana na adhabu au kulazimika kuwajibika, ili hata mambo ambayo Mungu anasema kuwahusu watendaji maovu hayataweza kuwahusu wao. Watu hawa hawako radhi kufahamu tabia ya Mungu, wamechoshwa na kujaribu kujua Mungu na kila kitu kuhusu Yeye. Wangependelea kwamba Mungu asiwepo. Watu hawa wanampinga Mungu na wao ndio watakaoondolewa.

Kisha, tutazungumzia hadithi ya Nuhu na namna ambavyo inahusiana na mada ya kazi ya Mungu, tabia ya Mungu na Mungu Mwenyewe.

Mnaona Mungu akimfanya nini Nuhu kwenye sehemu hii ya maandiko? Pengine kila mmoja aliyeketi hapa anajua kitu kuhusu hayo baada ya kusoma maandiko: Mungu alimfanya Nuhu kujenga safina, kisha Mungu akatumia gharika kuangamiza ulimwengu. Mungu alimruhusu Nuhu kujenga safina ili kuokoa familia yake ya wanane, kuwaruhusu kuweza kuishi, ili kuwa babu wa kizazi kifuatacho cha wanadamu. Sasa hebu tuyasome maandiko.

2. Nuhu

1) Mungu Anuia kuangamiza Ulimwengu kwa Gharika, Amwagiza Nuhu Kuijenga Safina

Mwa 6:9-14 Hivi ni vizazi vyake Nuhu: Nuhu alikuwa mtu mwenye haki na mtimilifu katika vizazi vyake, naye Nuhu alitembea na Mungu. Naye Nuhu akapata watoto watatu wa kiume, Shemu, Hamu, na Yafethi. Dunia pia ilikuwa potovu mbele za Mungu, nayo dunia ilijaa vurugu. Naye Mungu akaiangalia dunia, na, tazama, ilikuwa imepotoka; kwa sababu kila aliye na mwili alikuwa amejipotoshea njia yake duniani. Naye Mungu akasema kwake Nuhu, Mwisho wa wote walio na mwili umefika mbele Zangu; kwa kuwa dunia imejawa na vurugu kupitia kwao; na, tazama, nitawaangamiza pamoja na dunia. Ujitengenezee safina ya mbao wa mvinye; utatengeneza vyumba ndani ya safina, na uipake lami ndani na nje.

Mwa 6:18-22 Lakini na wewe nitaliimarisha agano Langu; na utaingia ndani ya safina, wewe, na wana wako, na mke wako, na wake zao wana wako pamoja na wewe. Na kwa kila kilicho na uhai chenye mwili, utawaleta wawili wa kila aina katika safina, kuwaweka hai pamoja nawe; watakuwa wa kiume na wa kike. Kila ndege arukaye kwa aina yake, na mifugo kwa aina yake, kila kinachotambaa duniani kwa aina yake, wawili wa aina yote watakuja kwa wewe, ili uwaweke hai. Na ujichukulie chakula cha kila aina kinacholika, nawe ukikusanye kwako; na kitakuwa kwa ajili ya chakula cha ninyi, na cha wao. Nuhu alifanya hivyo; kulingana na vyote ambavyo Mungu alimwamrisha, alifanya hivyo.

Je sasa mnaelewa kwa jumla Nuhu ni nani baada ya kuzisoma fahamu hizi? Nuhu ni mtu wa aina gani? Maandishi asilia ni: “Nuhu alikuwa mtu mwenye haki na mtimilifu katika vizazi vyake.” Kulingana na uelewa wa watu wa kisasa, mtu mwenye haki wakati huo wa nyuma alikuwa mtu wa aina gani? Mtu mwenye haki anafaa kuwa mtu mtimilifu. Je, mnajua kama mtu huyu mtimilifu ni mtimilifu machoni mwa binadamu au ni mtimilifu machoni mwa Mungu? Bila shaka mtu huyu mtimilifu ni mtu mtimilifu machoni mwa Mungu na wala si machoni mwa binadamu. Haya yote ni kweli! Hii ni kwa sababu binadamu ni kipofu na hawezi kuona, na Mungu tu ndiye anayeiangalia nchi nzima na kila mmoja wetu, Mungu pekee ndiye anayejua Nuhu ni mtu mtimilifu. Hivyo basi, mpango wa Mungu wa kuuangamiza ulimwengu kwa gharika ulianza pindi tu Alipomuita Nuhu.

Katika enzi hiyo, Mungu alinuia kumuita Nuhu ili kufanya kitu muhimu sana. Kwa nini ilikuwa lazima Afanye hivyo? Kwa sababu Mungu alikuwa na mpango kwa moyo Wake wakati huo. Mpango Wake ulikuwa kuangamiza ulimwengu kwa gharika. Kwa nini auangamize ulimwengu? Maandiko yanasema hivi: “Dunia pia ilikuwa potovu mbele za Mungu, nayo dunia ilijaa vurugu.” Mnaona nini kutoka kwenye kauli “dunia ilijaa vurugu”? Ni ajabu duniani wakati ulimwengu na watu wake wanapotoka kwa kupindukia, na ni hivi: “dunia ilijaa vurugu.” Katika lugha ya leo, “ilijaa vurugu” inamaanisha kila kitu kimechanganyika. Kwa binadamu,

inamaanisha kwamba katika nyanja zote za maisha hakuna mpangilio, na mambo yamejaa fujo kweli na ni magumu kudhibiti. Katika macho ya Mungu, inamaanisha watu wa ulimwengu wamepotoka sana. Wamepotoka hadi kiwango gani? Wamepotoka hadi kiwango ambacho Mungu hawezi tena kuvumilia kuangalia na hawezi tena kuwa na subira kuhusu hali hiyo. Wamepotoka hadi kiwango ambacho Mungu anaamua kuwaangamiza. Wakati Mungu alipoamua kuuangamiza ulimwengu, Alipanga kupata mtu wa kuijenga safina. Kisha Mungu akamchagua Nuhu kufanya kitu hicho, ambacho ni kumruhusu Nuhu kuijenga safina. Kwa nini Mungu alimchagua Nuhu? Katika macho ya Mungu, Nuhu ni mtu mwenye haki na haijalishi kile ambacho Mungu atamwagiza yeye kufanya, atafanya vivyohivyo. Hii inamaanisha atafanya chochote anachoambiwa kufanya na Mungu. Mungu alitaka kumtafuta mtu kama huyu ili afanye kazi na Yeye, kukamilisha kile alichokuwa amemwaminia kufanya, kuikamilisha kazi Yake hapa duniani. Hapo nyuma, kulikuwa na mtu mwingine kando na Nuhu ambaye angekamilisha kazi hiyo? Bila shaka la! Nuhu ndiye aliyekuwa mtu wa pekee ambaye angeweza kukamilisha kile ambacho Mungu alikuwa amemwaminia kufanya, na hivyo Mungu alimchagua yeye. Lakini je upana na viwango vya Mungu vya kuwaokoa watu hapo nyuma vilikuwa sawa na vile vya sasa? Jibu ni bila shaka kunayo tofauti! Na kwa nini Nauliza hili? Nuhu pekee ndiye aliyekuwa mwanadamu mwenye haki machoni pa Mungu wakati huo, ambalo linadokeza kwamba watoto wake wa kiume, na mke na wakwe wake wote hawakukuwa watu wenye haki, lakini Mungu bado aliwasamehe kwa sababu ya Nuhu. Mungu hakuwawekea matakwa kama Anavyofanya sasa, na badala yake Aliwaweka hai wanachama wote wanane wa familia ya Nuhu. Walipata baraka za Mungu kwa sababu ya Nuhu kuwa mwenye haki. Kama Nuhu asingekuwepo, hakuna yeyote kati yao ambaye angekamilisha kile ambacho Mungu alikuwa amemwaminia kufanya. Hivyo basi Nuhu alikuwa ndiye mtu wa pekee ambaye alitakikana kubakia hai baada ya ulimwengu kuangamizwa wakati huo, na wale wengine walikuwa tu wafadhiliwa wa ziada. Hii inaonyesha kwamba, katika enzi kabla ya Mungu kuanza rasmi kazi Yake ya usimamizi, kanuni na viwango ambavyo Alishughulikia watu na kuwadaai mahitaji vilikuwa vimelegezwa kidogo. Kwa watu wa leo, namna ambavyo Mungu alivyoshughulikia familia ya Nuhu ya watu wanane yaonekana kukosa haki. Lakini tukilinganisha na wingi wa kazi ambayo Yeye Anafanya kwa watu na kiwango cha neno Lake Analopitisha, namna Mungu alivyoshughulikia familia ya Nuhu ya watu wanane ilikuwa tu ni kanuni ya kazi Yake aliyoifanyia katika usuli wa kazi Yake wakati huu. Kwa kulinganisha, familia ya Nuhu ya watu wanane ndio ilipokea mengi zaidi kutoka kwa Mungu au ni watu wa Mungu ndio waliopokea?

Kwamba Nuhu aliitwa ni ukweli mdogo, lakini hoja kuu ya kile tunachozungumzia sasa—tabia ya Mungu, mapenzi Yake kiini Chake halisi katika rekodi hii—si rahisi. Ili kuelewa dhana hizi mbalimbali za Mungu lazima kwanza tuelewe ni mtu wa aina gani ambaye Mungu hutamani

kuita, nakupitia hii, tuweze kuelewa tabia yake, mapenzi yake na kiini chake halisi. Kufanya hivi ni muhimu. Hivyo katika macho ya Mungu, mtu huyu ni wa aina gani ambaye yeye humwita? Huyu lazima awe ni mtu anayeweza kuyasikiza maneno Yake. Wakati huohuo, lazima mtu huyu awe yule wa kuwajibika, mtu atakayetekeleza neno la Mungu kwa kuliona kuwa jukumu na wajibu ambao anahitajika kukamilisha. Basi mtu huyu anahitajika kuwa mtu anayemjua Mungu? La. Hapo nyuma, Nuhu hakuwa ameyasikia sana mafundisho ya Mungu wala kupitia kazi yoyote ile ya Mungu. Hivyo basi, maarifa ya Nuhu kumhusu Mungu yalikuwa madogo mno. Ingawaje imerekodiwa hapa kwamba Nuhu alitembea na Mungu, aliwahi kuiona nafsi ya Mungu? Jibu ni bila shaka la! Kwa sababu katika siku hizo, wajumbe wa Mungu tu ndio waliowaendea watu. Ingawa waliweza kuwakilisha Mungu katika kusema na kufanya mambo, walikuwa wakipitisha tu mapenzi na nia Zake. Nafsi ya Mungu haikufichuliwa kwa binadamu uso kwa macho. Kwenye sehemu hii ya maandiko, chote tunachoona tu ni kile ambacho mtu huyu Nuhu alilazimika kufanya na maagizo ya Mungu kwake yalikuwa gani. Hivyo basi ni kiini kipi kilichoonyeshwa na Mungu hapa? Kila kitu anachofanya Mungu kimepangiliwa kwa uhakika. Anapoonamba jambo au hali ikitokea, kutakuwa na kiwango cha kulipima jambo hilo katika macho Yake, na kiwango hiki kitaamua kama Ataanza mpango wa kulishughulikia au namna ya kuchukulia jambo na hali hii. Yeye anajali na ana hisia kwa kila kitu. Kwa hakika ni kinyume kabisa cha mambo. Kunao mstari hapa ambao Mungu alimwambia Nuhu: “Mwisho wa wote walio na mwili umefika mbele Zangu; kwa kuwa dunia imejawa na vurugu kupitia kwao; na, tazama, nitawaangamiza pamoja na dunia.” Katika maneno ya Mungu wakati huu, Alisema kwamba Angeangamiza binadamu tu? La! Mungu Alisema kwamba Angeangamiza viumbe wote hai wenye mwili. Kwa nini Mungu alitaka kuangamiza? Kunao ufunuo mwingine wa tabia ya Mungu hapa: Katika macho ya Mungu, kunayo mipaka ya subira yake kwa kupotoka kwa binadamu, kwa uchafu, vurugu, na kutotii kwa mwili wote. Mipaka Yake ni ipi? Ni kama vile alivyosema Mungu: “Mungu akaiangalia dunia, na, tazama, ilikuwa imepotoka; kwa sababu kila aliye na mwili alikuwa amejiipotoshea njia yake duniani.” Kauli hii “kwa sababu kila aliye na mwili alikuwa amejiipotoshea njia yake duniani” inamaanisha nini? Inamaanisha kiumbe yeyote hai, wakiwemo wale waliofuata Mungu, wale walioita jina la Mungu, wale waliowahi kutoa sadaka za kuteketezwa kwa Mungu, wale waliomtambua Mungu kwa vinywa vyao na hata kumsifia Mungu—pindi tabia yao ilipojaa upotovu na kufikia macho ya Mungu, basi ingemlazimu kuwaangamiza. Hiyo ndiyo ilikuwa mipaka ya Mungu. Hivyo basi ni hadi kiwango kipi Mungu alibakia kuwa mwenye subira kwa binadamu na upotovu wa mwili wote? Hadi katika kiwango ambacho watu wote, wawe wafuasi wa Mungu au wasioamini, walikuwa hawatembelei njia sahihi. Hadi kiwango ambacho binadamu alikuwa hajapotoshwa tu katika maadili na mwenye wingi wa maovu, lakini pia pale ambapo hakukuwa na mtu aliyesadiki uwepo wa Mungu, tupilia mbali yeyote aliyesadiki kuwa ulimwengu unatawaliwa na Mungu na kwamba Mungu anaweza

kuwaletea watu nuru na njia sahihi. Hadi kiwango ambacho binadamu aliudharau uwepo wa Mungu, na hakumruhusu Mungu kuwepo. Pindi upotovu wa mwanadamu ulipofikia kiwango hiki, Mungu asingeweza tena kuwa na subira Ni nini kingechukua nafasi yake? Kuja kwa hasira ya Mungu na adhabu ya Mungu. Huu haukuwa ufunuo kiasi wa tabia ya Mungu? Katika enzi hii ya sasa, yupo bado binadamu mwenye haki katika macho ya Mungu? Yupo bado binadamu mtimilifu katika macho ya Mungu? Enzi hii ndiyo ile ambayo tabia ya miili yote duniani imepotoka mbele ya macho ya Mungu? Katika siku na enzi hii, mbali na wale Mungu anataka kuwafanya kuwa kamili, wale wanaoweza kumfuata Mungu na kuukubali wokovu Wake, huoni kwamba watu wote wa mwili wanapatia changamoto ile mipaka ya subira ya Mungu? Si kila kitu kinachofanyika kando yenu, kila mnachooni kwa macho yenu, na kusikia kwa masikio yenu, na kupitia ninyi binafsi kila siku katika ulimwengu huu kimejaa vurugu? Katika macho ya Mungu, si ulimwengu kama huu, enzi kama hii, inafaa kukomeshwa? Ingawaje usuli wa enzi ya sasa ni tofauti kabisa na usuli wa enzi ya Nuhu, hisia na hasira Alizo nazo Mungu kwa kupotoka kwa binadamu inabakia ileile sawa na ilivyokuwa wakati huo. Mungu anaweza kuwa mwenye subira kwa sababu ya kazi Yake, lakini kulingana na hali na masharti ya aina yote, ulimwengu huu unafaa kuwa uliangamizwa kitambo katika macho ya Mungu. Hali imepita na kupitiliza ile iliyokuwa hapo nyuma wakati ulimwengu uliangamizwa na gharika. Lakini tofauti ni nini? Hili ndilo jambo jingine linalohuzunisha moyo wa Mungu zaidi, na pengine kitu ambacho hakuna yeyote kati yenu anaweza kutambua.

Alipokuwa akiuangamiza ulimwengu kwa gharika, Mungu angemwita Nuhu ili kuijenga safina na kufanya baadhi ya kazi ya matayarisho. Mungu angemwita binadamu mmoja—Nuhu—kumfanyia misururu hii ya mambo. Lakini kwenye enzi ya sasa, Mungu hana mtu yeyote wa kumuita. Kwa nini hivyo? Kila mmoja aliyeketi hapa pengine anaelewa na kujua sababu vizuri sana. Je, mngependa Mimi niweze kuiweka wazi? Kuitaja kwa sauti huenda kukawaaibisha na kufanya kila mmoja kukasirika. Baadhi ya watu wanaweza kusema: “Ingawaje sisi si watu wenye haki na wala sisi si watu watimilifu kwenye macho ya Mungu, kama Mungu atatuelekeza sisi kufanya kitu, bado tutaweza kukifanya. Kabla, Aliposema janga kuu lilikuwa likija, tulianza kutayarisha chakula na vitu ambavyo tungehitaji wakati wa janga hilo. Si haya yote yalifanywa kulingana na mahitaji ya Mungu? Si tulikuwa tukishirikiana kwa hakika na kazi ya Mungu? Mambo haya tuliyofanya hayawezi kulinganishwa na kile Nuhu alifanya? Kwani kufanya kile tulichofanya si utiifu wa kweli? Kwani hatukuwa tunafuata maagizo ya Mungu? Kwani hatukufanya kile Mungu alichosema kwa sababu tunayo imani katika maneno ya Mungu? Basi kwa nini Mungu angali na huzuni? Kwa nini Mungu anasema Hana mtu wa kumwita?” Kunao tofauti wowote kati ya vitendo vyenu na vile vya Nuhu? Tofauti ni nini? (Kutayarisha chakula leo kwa minajili ya janga kulikuwa nia yetu binafsi.) (Matendo yetu hayawezi kufikia yale ya

“haki,” ilhali Nuhu ni mtu mwenye haki mbele ya macho ya Mungu.) Kile mlichosema hakiko mbali sana na ukweli. Kile alichofanya Nuhu ni tofauti sana kulingana na kile watu wanafanya sasa. Wakati Nuhu alipofanya kama vile Mungu alivyomwagiza hakujua nia za Mungu zilikuwa nini. Hakujua ni nini ambacho Mungu Alitaka kukamilisha. Mungu alikuwa amempa tu amri, Akamwagiza afanye kitu, lakini bila ya maelezo mengi, na akaendelea mbele na kukifanya. Hakujaribu kuelewa kwa siri nia za Mungu zilikuwa nini, wala hakumpinga Mungu au kuwa na fikira mbili kuhusu jambo hilo. Alienda tu na kuifanya vilivyo kwa moyo safi na rahisi. Chochote ambacho Mungu alimruhusu kufanya alifanya, na kutii na kusikiliza neno la Mungu vyote vilikuwa ni imani yake ya kufanya mambo. Hivyo ndivyo alivyokuwa mnyofu na mwepesi wa kushughulikia kile ambacho Mungu alimwaminia kufanya. Kiini chake—kiini cha vitendo vyake kilikuwa ni utiifu, sio kutarajia kwa kukisia, sio kupinga, na zaidi; kutofikiria kuhusu maslahi yake binafsi na faida zake na hasara zake. Zaidi ya hayo, wakati Mungu aliposema Angeuangamiza ulimwengu kwa mafuriko, Nuhu hakuuliza ni lini au kuuliza kile kitakachovifanyikia vitu, na bila shaka hakumuuliza Mungu namna hasa alivyopanga kuangamiza ulimwengu. Alifanya tu kama Mungu alivyomwagiza. Njia yoyote ile aliyotaka Mungu, safina hiyo iweze kujengwa na hasa kujengwa na nini, alifanya tu vile ambavyo Mungu alimwomba na pia akaanza kazi mara moja. Alitenda kulingana na maagizo ya Mungu kwa mwelekeo wa kutaka kutosheleza Mungu. Je, alikuwa akifanya hivyo kujisaidia yeye kuepuka janga? La. Je, alimwuliza Mungu ni baada ya muda gani zaidi kabla ulimwengu ungeangamizwa? Hakuuliza. Je, alimwuliza Mungu au alijua ingechukua muda gani kuijenga safina? Hakujua hilo pia. Alitii tu, akasikiliza, na kufanya hivyo inavyohitajika. Watu wa sasa si sawa: Pindi tu taarifa fulani inapojitokeza kupitia kwa neno la Mungu, pindi tu watu wanapohisi ishara ya kutatizwa au matatizo, wote watachukua hatua mara moja, haijalishi ni nini, au gharama husika, ili kutayarisha kile ambacho watakula, kunywa, na kutumia athari za baadaye, hata kupanga njia za wao kutoroka wakati janga litakapovamia. Hata ya kuvutia zaidi ni kwamba, wakati huu muhimu, akili za binadamu zinakuwa zenye “manufaa sana.” Katika hali ambazo Mungu hajanipa maagizo yoyote, binadamu anaweza kupanga kila kitu kwa njia inayofaa Mngeweza kutumia neno “sahihi” ili kuielezea. Na kuhusiana na kile Mungu anachosema, nia za Mungu ni nini, au kile Mungu anataka ni nini, hakuna anayejali na hakuna anayejaribu kukitambua. Je, hii siyo tofauti kubwa zaidi kati ya watu wa leo na Nuhu?

Katika rekodi hii ya hadithi ya Nuhu, mnaona sehemu ya tabia ya Mungu? Kunacho mpaka kwa subira ya Mungu kwa upotovu, uchafu, na vurugu la binadamu. Anapofikia ule mpaka, Hatawahi tena kuwa na subira na badala yake Atanza usimamizi Wake mpya na mpango mpya, kuanza kufanya kile ambacho lazima Afanye, kufichua matendo Yake na upande ule mwingine wa tabia Yake. Kitendo hiki Chake si cha kuonyesha kwamba lazima Asiwahi kukosewa na

binadamu au kwamba Yeye amejaa mamlaka na hasira, na wala si kuonyesha kwamba Anaweza kuangamiza binadamu. Ni kwamba tabia Yake na kiini chake takatifu ambacho hakiwezi tena kuruhusu, hakina tena subira kwa aina hii ya binadamu kuishi mbele Yake, kuishi chini ya utawala Wake. Hivyo ni kusema, wakati wanadamu wote wako dhidi Yake, wakati hakuna mtu yeyote Anayeweza kuokoa katika ulimwengu mzima, Hatakuwa tena na subira kwa binadamu kama hawa, na Ataweza, bila ya utundu wowote, kutekeleza mpango Wake—kuangamiza binadamu wa aina hii. Kitendo kama hicho cha Mungu kinaamuliwa na tabia Yake. Hii ni athari inayohitajika, na athari ambayo kila kiumbe aliyeumbwa chini ya utawala wa Mungu lazima ashuhudie. Je, haya hayaonyeshi kwamba katika enzi ya sasa, Mungu hawezi kusubiri kukamilisha mpango Wake na kuokoa watu Anaotaka kuokoa? Katika hali hizi, Mungu anajali kuhusu nini zaidi? Si vile wale wasiomfuata Yeye kabisa au wale wanaompinga Yeye kwa vyovyote vile wanamshughulikia Yeye au kumpinga Yeye, au namna ambavyo mwanadamu anamdaganya Yeye. Anajali tu kuhusu kama wale wanaomfuata Yeye, walengwa wa wokovu Wake katika mpango Wake wa usimamizi, wamewekwa kamili na Yeye, na kama wametimiza utoshelezi Wake. Kuhusiana na watu wale wengine bali na wale wanaomfuata Yeye, Anawatolea tu adhabu kidogo mara kwa mara ili kuonyesha ghadhabu Yake. Kwa mfano tsunami, mitetemeko ya ardhi, kuibuka kwa volkano na kadhalika. Wakati huohuo, Anawalinda kwa dhati na kuwashughulikia wale wanaomfuata Yeye na karibu wanaokolewa na Yeye. Tabia ya Mungu ni hii: Kwa mkono mmoja, Anaweza kuwapatia watu Anaonua kutekeleza subira na ustahimilivu kamili wa kupindukia na kuwasubiria wao kwa muda mrefu Anavyoweza; kwa mkono mwingine, Mungu anachukia na kuchukizwa kwa dhati na watu wa aina ya Shetani wasiomfuata Yeye na wanaompinga Yeye. Ingawaje Hajali kama hawa watu wa aina ya Shetani wanamfuata au wanamwabudu Yeye, bado Anawachukia wao huku akiwa na subira na wao katika moyo Wake, na Anapoamua mwisho wa hawa watu wa aina ya Shetani, Yeye pia anasubiria kufika kwa hatua za mpango Wake wa usimamizi.

Hebu tuangalie kifungu kinachofuata.

2) Baraka za Mungu kwa Nuhu Baada ya Gharika

Mwa 9:1-6 Naye Mungu akawabariki Nuhu na wana wake, na akasema kwao, Ninyi Zaeni, na muongezeke, na muijaze tena dunia. Na wanyama wote wa dunia watawaogopa na kuwa na hofu nanyi, na ndege wote wa angani, na vyote vitembeavyo duniani, na kila samaki wa baharini; wamewekwa katika mikono yenu. Kila kisongacho kilicho na uhai kitakuwa chakula chenu, jinsi ambavyo nimewapa mboga ndivyo ninavyowapa vitu vyote. Lakini nyama iliyo na uhai, ambayo ni damu yake, ninyi msiile. Na bila shaka nitahitaji damu yenu ya uhai wenu, nitahitaji kwa mkono wa kila mnyama, na kwa mkono wa mwanadamu, nitahitaji uhai wa mwanadamu kwa

mkono wa ndugu wa kila mwanadamu. Yeyote ambaye atamwaga damu ya mwanadamu, damu yake itamwagika na mwanadamu: kwa kuwa Mungu alimfanya mwanadamu kwa mfano Wake.

Ni nini mnachoona katika kifungu hiki? Kwa nini Nikachagua mistari hii? Kwa nini Sikuchukua dondoo la Nuhu na maisha ya familia yake kwenye safina? Kwa sababu maelezo haya hayana muunganisho mwingi na mada ambayo tunawasiliana leo. Kile tunachotilia maanani ni tabia ya Mungu. Kama mnataka kujua kuhusu maelezo hayo, basi mnaweza kuchukua Biblia ili muweze kujisomea mwenyewe. Hatutaizungumzia hiyo hapa. Kitu kikuu tunachozungumzia leo ni kuhusu namna ya kujua matendo ya Mungu.

Baada ya Nuhu kukubali maagizo ya Mungu na kujenga safina na kuishi katika siku zile husika Mungu alitumia gharika ili kuangamiza ulimwengu, familia yake nzima ya wanane ilinusurika. Mbali na familia ya Nuhu ya wanane, wanadamu wote waliangamizwa, na viumbe wote nchini wakaangamizwa. Kwa Nuhu, Mungu alimpa baraka, na akasema baadhi ya mambo kwake na watoto wake wa kiume. Mambo haya yalikuwa yale ambayo Mungu alikuwa akimpa yeye na pia baraka zake kwake yeye. Hizi ndizo baraka na ahadi Mungu humpa yule ambaye anaweza kumsikiliza Yeye na kuyakubali maagizo Yake, na pia namna anavyotuzwa watu. Hivi ni kusema, haijalishi kama Nuhu alikuwa binadamu mtimilifu au alikuwa binadamu mwenye haki mbele ya macho ya Mungu, na haijalishi ni kiwango kipi alichomjua Mungu, kwa ufupi, Nuhu na watoto wake wa kiume watatu wote waliyasikiliza maneno ya Mungu, wakaratiwa na kazi ya Mungu, na kufanya kile walichofaa kufanya kulingana na maagizo ya Mungu. Kutokana na hayo, walimsaidia Mungu kuweza kubakiza binadamu na aina mbalimbali za viumbe walio na uhai baada ya kuangamizwa kwa ulimwengu na gharika, na hivyo wakawa wamefanya mchango mkubwa kwa hatua iliyofuata ya mpango wa usimamizi wa Mungu. Kwa sababu ya kila kitu alichokuwa amefanya, Mungu alimbariki. Pengine kwa watu wa leo, kile alichofanya Nuhu hakikuwa sana na thamani ya kutajwa. Baadhi wanaweza hata kufikiria: Nuhu hakufanya chochote; Mungu alikuwa ameamua akilini Mwake kumhifadhi, hivyo kwa hakika angehifadhiwa. Kuwepo kwake si kwa sababu yake. Hili ndilo jambo ambalo Mungu alitaka lifanyike, kwa sababu binadamu ni mtulivu. Lakini hicho sicho Mungu alikuwa anafikiria. Kwa Mungu, haijalishi kama mtu ni mkubwa au asiye wa maana, mradi tu aweze kumsikiliza Yeye, kutii maagizo Yake na kile anachomwaminia na aweze kushirikiana na kazi Yake, mapenzi Yake, na mpango Wake, ili mapenzi Yake na Mpango Wake iweze kukamilika vizuri, basi mwenendo wake unastahili kukumbukwa na Yeye na kustahili kupokea baraka Zake. Mungu huthamini sana watu kama hao, na Yeye Hupenda sana vitendo vyao na upendo wao na huba yao Kwake. Huu ndio mwelekeo wa Mungu. Hivyo kwa nini Mungu alimbariki Nuhu? Kwa sababu hivi ndivyo Mungu anavyoshughulikia vitendo kama hivyo na utiifu wa mwanadamu.

Kuhusiana na baraka za Mungu kwa Nuhu, baadhi ya watu watasema: “Kama binadamu atamsikiliza Mungu na kumtosheleza Mungu, basi Mungu anafaa kumbariki binadamu. Je, hilo halifanyiki hivyo bila kusema?” Tunaweza kusema hivyo? Baadhi ya watu husema: “La.” Kwa nini hatuwezi kusema hivyo? Baadhi ya watu husema: “Binadamu hastahili kufurahia baraka za Mungu.” Hilo si sahihi kabisa. Kwa sababu wakati mtu anapokubali kile Mungu amemwaminia, Mungu anacho kiwango cha kuhukumu kama vitendo vya mtu huyu ni vizuri au vibaya na kama mtu huyu amemtii, na kama mtu huyu ametosheleza mapenzi ya Mungu na kama kile anachofanya kimeruhusiwa. Kile anachojali Mungu ni kuhusu moyo wa mtu huyu, si vitendo vyake vya juujuu. Si jambo kwamba Mungu anafaa kubariki mtu mradi tu afanye hivyo, licha ya namna anavyofanya hivyo. Huku ni kutoelewa kwa watu kumhusu Mungu. Mungu huangalia tu mwisho wa matokeo ya mambo, lakini Anatilia mkazo zaidi kuhusu namna moyo wa mtu ulivyo na namna mwelekeo wa mtu ulivyo wakati wa maendeleo ya mambo, na Anaangalia kama kuna utiifu, utiliaji maanani, na tamani ya kumtosheleza Mungu ndani ya moyo wake. Nuhu alijua kiasi kipi kumhusu Mungu wakati huo? Kiasi hicho kilikuwa kingi kama mafundisho ya dini mnayojua sasa? Kuhusu dhana za ukweli kama vile dhana na maarifa ya Mungu, alipokea kunyunyizia na uchungaji kama ninyi? La, hakupokea! Lakini kuna ukweli mmoja ambao haupingiki: Katika fahamu, akili, na hata kina cha mioyo ya watu wa leo, dhana zao na mwelekeo wao kwa Mungu umejaa ukungu na haeleweki. Mnaweza hata kusema kwamba sehemu fulani ya watu inashikilia mwelekeo mbaya kwa uwepo wa Mungu. Lakini katika moyo wa Nuhu na fahamu yake, uwepo wa Mungu ulikuwepo na bila shaka, na hivyo basi utiifu wake kwa Mungu ulikuwa haujatiwa doa wala toa na ungeweza kustahimili majaribio. Moyo wake ulikuwa safi na wazi kwa Mungu. Hakuhitaji maarifa ya mafundisho ya dini mengi mno ili kujishawishi kufuata kila neno la Mungu, wala hakuhitaji ukweli mwingi kuthibitisha uwepo wa Mungu, ili akubali kile Mungu alimwaminia na kuweza kufanya chochote kile ambacho Mungu angemruhusu kufanya. Hii ni tofauti muhimu kati ya Nuhu na watu wa leo, na pia ndio ufasili wa kweli hasa kuhusu binadamu mtimilifu alivyo machoni mwa Mungu. Kile anachotaka Mungu ni watu kama Nuhu. Yeye ni aina ya mtu anayesifiwa na Mungu, na pia hasa mtu wa aina ile ambaye Mungu hubariki. Mmepokea nuru yoyote kutoka haya? Watu huangalia watu kutoka nje, huku naye Mungu anaangalia mioyo ya watu na kiini chao. Mungu hamruhusu yeyote kuwa na moyo wowote wa kukosa ari au shaka kwake Yeye, wala Hawaruhusu watu kushuku au kumjaribu Yeye kwa njia yoyote ile. Hivyo, ingawaje watu wa leo wako uso kwa uso na neno la Mungu, au mnaweza hata sema kwamba wako uso kwa uso na Mungu, kutokana na kitu kilicho ndani ya mioyo yao, uwepo wa kiini chao potovu, na mwelekeo wao wenye ukatili kwake Yeye, wamezuiliwa kutoka kwa imani yao ya kweli kwa Mungu na kuzibwa kutoka kwa utiifu wao kwake Yeye. Kwa sababu ya haya, ni vigumu sana kwao kutimiza baraka sawa ambazo Mungu alikabidhi Nuhu.

3) Mungu Atumia Upinde wa Mvua Kama Ishara ya Agano Lake na mwanadamu

Mwa 9:11-13 Na nitaweka agano Langu na ninyi, wala miili yote haitaondolewa tena na maji ya gharika; wala hakutakuwa na gharika tena kuiharibu dunia. Naye Mungu akasema, Hii ni alama ya agano ambayo naifanya kati ya Mimi na ninyi na viumbe vyote vyenye uhai vilivyo nanyi, kwa vizazi vya kudumu: naweka upinde Wangu mawinguni, na utakuwa alama ya agano kati ya Mimi na dunia.

Kisha, hebu tuangalie sehemu hii ya maandiko kuhusu namna Mungu alivyounda upinde wa mvua kama ishara ya Agano lake na binadamu.

Watu wengi zaidi wanajua upinde wa mvua ni nini na wamesikia baadhi ya hadithi zinazohusiana na pinde za mvua. Kuhusiana na hadithi ile ya upinde wa mvua kwenye biblia, baadhi wa watu wanaisadiki, baadhi wanaichukulia tu kama hadithi ya kale, huku wengine hawaisadiki kamwe. Haijalishi ni nini, kila kitu kilichofanyika kuhusiana na upinde wa mvua ndicho kila kitu ambacho Mungu Alifanya hapo awali, na mambo yaliyofanyika katika mchakato huu wa usimamizi wa Mungu wa binadamu. Mambo haya yamerekodiwa vivyo hivyo kwenye Biblia. Rekodi hizi hazituambii chochote kuhusu hali ya Mungu ilivyokuwa wakati huo au nia zake nyuma ya maneno haya ambayo Mungu alisema. Zaidi, hakuna anayeweza kutambua ni nini Mungu alikuwa akihihi Aliposema maneno hayo. Hata hivyo, hali ya akili ya Mungu kuhusiana na hiki kitu chote inafichuliwa katikati ya mistari ya maandishi. Ni kana kwamba fikira zake wakati huo zinatoka kwenye ukurasa kupitia kila neno na kauli ya neno la Mungu.

Fikira za Mungu ni kile ambacho watu wanafaa kujali kuhusu na kile wanafaa kujaribu kujua zaidi. Hii ni kwa sababu fikira za Mungu zinahusiana kwa karibu na uelewa wa binadamu wa Mungu na uelewa wa binadamu wa Mungu ni kiungo muhimu sana kwa kuingia kwa binadamu katika maisha. Hivyo ni nini alichokuwa akifikiria Mungu wakati huo mambo haya yalipofanyika?

Hapo mwanzo, Mungu aliumba binadamu ambao katika macho Yake walikuwa wazuri sana na karibu na Yeye, lakini waliangamizwa na gharika baada ya kuasi dhidi Yake. Je, ilimwumiza Mungu kwamba binadamu kama hao walitoweka tu papo hapo hivyo? Bila shaka Aliumizwa! Kwa hivyo Maonyesho Yake ya maumivu haya yalikuwa nini? Ilirekodiwa vipi kwenye Biblia? Ilirekodiwa kwenye Biblia kama: “Na nitaweka agano langu na ninyi, wala miili yote haitaondolewa tena na maji ya gharika; wala hakutakuwa na gharika tena kuiharibu dunia.” Sentensi hii rahisi inafichua fikira za Mungu. Kuangamizwa huku kwa ulimwengu kulimpa Yeye maumivu sana. Kwa maneno ya binadamu, Alikuwa na huzuni sana. Tunaweza kufikiria: Ni vipi ambavyo dunia iliyokuwa imejaa maisha inavyofanana baada ya kuangamizwa na gharika? Ni

vipi ambavyo dunia iliyokuwa imejaa binadamu inavyofanana hivi sasa? Hakuna makazi ya binadamu, hakuna viumbe walio hai, maji kila mahali na machafuko kabisa juu ya maji. Hilo ndilo lililokuwa onyesho la kusudio la asili ya Mungu wakati alipoumba ulimwengu? Bila shaka la! Nia asilia ya Mungu ilikuwa ni kuyaona maisha katika maeneo yote, kuwaona wanadamu Aliowaumba wakimwabudu Yeye, si tu kwa Nuhu kuwa mtu pekee anayemwabudu, au kuwa wa pekee ambaye angejibu mwito Wake ili kukamilisha kile alichoumba awali lakini kinyume cha mambo. Ni vipi ambavyo moyo Wake usingekuwa katika maumivu? Hivyo Alipokuwa akifichua tabia Yake na kuelezea hisia Zake, Mungu alifanya uamuzi. Ni aina gani ya uamuzi Alifanya? Kuunda uta mawinguni (kumbuka: upinde wa mvua tunaouona) kama agano na binadamu, ahadi kwamba Mungu hangemwangamiza mwanadamu kwa gharika tena. Wakati huohuo, ulikuwa pia ni kuwaambia watu kwamba Mungu aliwahi kuangamiza ulimwengu kwa gharika, kumfanya mwanadamu kukumbuka milele ni kwa nini Mungu alifanya kitu kama hicho.

Je, kuangamizwa kwa ulimwengu wakati huu kulikuwa ni jambo alilotaka Mungu? Bila shaka lilikuwa ni jambo asilotaka Mungu Huenda tukaweza kufikiria sehemu ndogo ya picha ile ya kusikitikia ya ulimwengu baada ya kuangamizwa kwa ulimwengu lakini hatuwezi kukaribia kufikiria namna hali ilivyokuwa wakati huo mbele ya macho ya Mungu. Tunaweza kusema kwamba, haijalishi kama ni watu wa sasa au wa wakati huo, hakuna yeyote anayeweza kufikiria au kutambua ni vipi Mungu alikuwa akihihi Aliposhuhudia tukio hilo, picha hiyo ya ulimwengu baada ya kuangamizwa kwake kwa gharika. Mungu alilazimishwa kufanya haya kutokana na kutotii kwa binadamu, lakini maumivu ambayo moyo wa Mungu ulipitia kutokana na maangamizo haya ya ulimwengu kwa gharika ni uhalisia ambao hakuna anayeweza kuufikiria au kuutambua. Ndiyo maana Mungu aliweka agano na mwanadamu, ambalo lilikuwa ni kuambia watu kukumbuka kwamba Mungu aliwahi kufanya kitu kama hiki, na kuapa kwamba Mungu asingewahi kuangamiza ulimwengu kwa njia hii tena. Katika agano hili, tunauona moyo wa Mungu—tunaona kwamba moyo wa Mungu ulikuwa katika maumivu Alipoangamiza binadamu hawa. Katika lugha ya binadamu, wakati Mungu aliangamiza mwanadamu na Akaona mwanadamu akitoweka, moyo Wake ulikuwa ukiomboleza na kuvuja damu. Je, hivyo sivyo tunavyoweza kuifafanua kwa njia bora zaidi? Maneno haya yanatumika na binadamu kuonyesha hisia za binadamu, lakini kwa sababu lugha ya binadamu inao ukosefu mwingi, kuitumia kufafanua hisia za Mungu hakuonekani kuwa mbaya sana kwangu Mimi, na wala si kubwa mno. Angaa inawapa uelewa sahihi kabisa, wa kufaa zaidi, wa hali ya Mungu ilivyokuwa wakati huo. Sasa mtafikiria nini mtakapouona upinde wa mvua tena? Angaa mtakumbuka namna ambavyo Mungu aliwahi kuwa katika huzuni kwa sababu ya kuangamiza ulimwengu kwa gharika. Mtakumbuka namna, hata kama Mungu aliuchukia ulimwengu huu na kudhalilisha binadamu

hawa, Alipowaangamiza wanadamu Alioumba kwa mikono Yake mwenyewe, moyo Wake ulikuwa ukisononeka, ukipambana kuachilia, ukihisi kusita, na kuhisi vigumu kuvumilia mambo. Tulizo lake pekee lilikuwa katika familia ya wanane ya Nuhu. Ulikuwa ni ushirikiano wa Nuhu uliofanya jitihada Zake za kipekee za kuumba viumbe wote kuwa cha thamani. Kwa wakati ambao Mungu alikuwa akiteseka, hili ndilo jambo tu ambalo lingeweza kusawazisha maumivu Yake. Kuanzia hapo, Mungu aliweka matarajio Yake yote ya binadamu kwa familia ya Nuhu, akitumai kwamba wangeishi chini ya baraka Zake na si laana Yake, akitumai kwamba wasingewahi kumwona Mungu akiuamamiza ulimwengu kwa gharika na pia akitumai kwamba wasingeamamizwa.

Ni sehemu gani ya tabia ya Mungu tunayofaa kuelewa kutoka hapa? Mungu alikuwa amemdharau binadamu kwa sababu binadamu alikuwa na uadui na Yeye, lakini ndani ya moyo Wake, utunzaji Wake, kujali Kwake, na huruma Yake kwa binadamu vilibakia vilevile. Hata wakati alipowaangamiza wanadamu, moyo Wake hukubadilika. Wakati binadamu walikuwa wamejaa upotovu na kutotii Mungu hadi katika kiwango fulani, Mungu alilazimika, kwa sababu ya tabia Yake na kiini Chake, na kulingana na kanuni Zake, kuangamiza binadamu hao. Lakini kwa sababu ya kiini cha Mungu, bado Alisikitikia binadamu, hata Akataka kutumia njia mbalimbali za kuwakomboa wanadamu ili waweze kuendelea kuishi. Badala yake, binadamu alimpinga Mungu, akaendelea kutomtii Mungu, na kukataa kukubali wokovu wa Mungu, yaani, alikataa kukubali nia Zake nzuri. Haijalishi ni vipi Mungu aliwaita wao, aliwakumbusha, akawatosheleza haja zao, akawasaidia wao, au akawavumilia wao, binadamu hakutambua haya, wala hakutilia maanani. Katika maumivu Yake, Mungu bado hakusahau kumpa binadamu uvumilivu Wake wa kiwango cha juu zaidi, akisubiri binadamu kugeuka na kubadilika. Baada ya Yeye kufikia kikomo Chake, Alifanya kile Alicholazimika kufanya bila ya kusita. Kwa maneno mengine, kulikuwa na kipindi cha muda mahususi na mchakato kutoka pale ambapo Mungu alipanga kuangamiza wanadamu hadi katika mwanzo rasmi wa kazi Yake ya kuwaangamiza wanadamu. Mchakato huu ulikuwepo kwa kusudio la kumwezesha binadamu kugeuka, na ndio uliokuwa fursa ya mwisho ya Mungu kumpa binadamu. Hivyo ni nini ambacho Mungu alifanya kwenye kipindi hiki kabla ya kuangamiza wanadamu? Mungu alifanya kiwango kikubwa cha kazi ya kukumbusha na kazi ya kusihi. Haijalishi ni maumivu kiasi kipi na huzuni ambayo ilikuwa ndani ya moyo wa Mungu, Aliendelea kufanyisha zoezi utunzaji Wake, wasiwasi, na huruma nyingi juu ya binadamu. Tunaona nini kutoka kwa haya? Bila shaka, tunaona kwamba upendo wa Mungu kwa wanadamu ni wa kweli na si tu jambo ambalo Analizungumzia tu bila matendo. Ni jambo hakika, linaloweza kushikika na kutambulika, si bandia, halijatiwa najisi, halidanganyi wala halisingizii. Mungu kamwe hatumii uongo au kuunda taswira za bandia ili kufanya watu kuona kwamba Yeye anapendeka. Kamwe hatumii ushuhuda wa uongo ili

kuwafanya kuona uzuri Wake, au kuringia uzuri wake na utakatifu Wake. Je, dhana hizi za tabia ya Mungu zinastahili upendo wa binadamu? Kwani nazo hazistahili kuabudiwa? Kwani nazo hazistahili kupendwa sana? Kwa sasa, Ningependa kuwauliza: Baada ya kuyasikia maneno haya, mnafikiri kwamba ukubwa wa Mungu ni maneno matupu tu kwenye kipande cha karatasi? Je, uzuri wake Mungu ni maneno matupu tu? La! Bila shaka la! Mamlaka ya juu, ukubwa, utakatifu, uvumilivu, upendo, wa Mungu na kadhalika—kila utondoti wa kila mojawapo ya vipengele vya tabia ya Mungu na kiini Chake unapata maonyesho ya vitendo kila wakati Anapoanza kazi Yake, zikiwa katika mapenzi Yake kwa binadamu, na pia zikitimizwa na kuonyeshwa kwa kila mtu. Licha ya kama umewahi kuzihisi awali, Mungu anamtunza kila mtu katika kila njia inayowezekana, kwa kutumia moyo Wake wa dhati, hekima, na mbinu mbalimbali ili kupashana mioyo ya kila mtu, na kuzindua roho ya kila mmoja. Huu ni ukweli usiopingika. Haijalishi ni watu wangapi wameketi hapa, kila mtu amekuwa na uzoefu tofauti na hisia tofauti kwa ustahimilivu, uvumilivu, na uzuri wake Mungu. Uzoefu huu wote wa Mungu na hisia hizi au utambuzi wa Yeye—kwa ufupi, mambo haya yote mazuri yanatoka kwa Mungu. Hivyo kwa kutangamanisha uzoefu wa kila mmoja na maarifa ya Mungu na kuziweka kwa pamoja na masomo yetu ya vifungu hivi vya Biblia leo, je sasa unao uelewa halisi na bora zaidi kumhusu Mungu?

Baada ya kuisoma hadithi hii na kuelewa baadhi ya tabia za Mungu zilizofichuliwa kupitia kwa hafla hii, ni aina gani mpya kabisa ya shukrani mliyo nayo kwa Mungu? Je, imewapa uelewa wa kina zaidi wa Mungu na moyo Wake? Mnahisi tofauti sasa mnapoiangalia hadithi ya Nuhu tena? Kulingana na maoni yenu, ingehitajika kufanya mawasiliano ya mistari hii ya Biblia? Kwa vile tumewasiliana kuihusu, mnafikiria kwamba ilihitajika? Ilihitaika, siyo? Ingawaje kile tulichosoma ni hadithi, ni rekodi ya kweli ya kazi ya Mungu ambayo aliwahi kuifanya. Nia yangu haikuwa kuwawezesha kufahamu maelezo ya hadithi hizi au mhusika huyu, wala haikuwa kwamba mweze kuenda kusomea kuhusu mhusika huyu, na bila shaka si eti mweze kurudi katika uchambuzi wa Biblia tena. Mnaelewa? Hivyo, hadithi hizi zimesaidia maarifa yenu ya Mungu? Hadithi hii imeongezea nini uelewa wenu wa Mungu? Twambie, kina kaka na kina dada kutoka Hong Kong. (Tuliona kwamba upendo wa Mungu ni kitu ambacho hakuna yeyote kati yetu binadamu potovu anamiliki.) Twambie, akina kaka na akina dada kutoka Korea Kusini. (Upendo wa Mungu kwa binadamu ni wa kweli. Upendo wa Mungu kwa binadamu unao tabia Yake na unabeba ukuu Wake, utakatifu, uongozi, na ustahimilivu Wake. Inafaa sisi tujaribu kupata uelewa wa kina zaidi.) (Kupitia kwa mawasiliano ambayo tumetoka kuwa nayo, kwa upande mmoja Ninaweza kuona haki ya Mungu na tabia ya kitakatifu, na Ninaweza pia kuona wasiwasi alionao Mungu kwa mwanadamu, rehema za Mungu kwa mwanadamu, na kwamba kila kitu anachofanya Mungu na kila fikira na wazo Alilionalo linafichua upendo na kujali Kwake kwa

binadamu.) (Uelewa wangu katika siku zilizopita ulikuwa kwamba Mungu alitumia gharika kuangamiza ulimwengu kwa sababu mwanadamu alikuwa amegeuka na kuwa mwovu kwa kiwango fulani, na ilikuwa ni kana kwamba Mungu aliangamiza binadamu hawa kwa sababu Aliuchukia. Ilikuwa tu baada ya Mungu kuzungumza kuhusu hadithi ya Nuhu leo na Akasema ya kwamba moyo wa Mungu ulikuwa unavuja ndipo Ninatambua kwamba Mungu alikuwa kwa hakika shingo upande kuachilia binadamu hawa. Ilikuwa tu ni kwa sababu mwanadamu alikuwa mtovu wa kusikia sana kiasi cha kwamba Mungu alikuwa hana chaguo lakini kumwangamiza. Kwa hakika, moyo wa Mungu wakati huo ulikuwa umesikitika sana. Kutokana na haya Ninaweza kuona katika tabia ya Mungu utunzaji na kujali Kwake kwa mwanadamu. Hili ni jambo ambalo Sikulijua awali.) Vizuri sana! Mnaweza kwenda kwa kifuatacho. (Niliathiriwa sana baada ya kusikiliza. Nimeisoma Biblia kitambo, lakini sijawahi kuwa na uzoefu kama leo pale ambapo Mungu anachambua kwa njia ya moja kwa moja mambo haya ili tuweze kumjua Yeye. Kwa Mungu kutushika mkono kuweza kuona Biblia inanifanya nijue kwamba kiini cha Mungu kabla ya kupotoshwa kwa binadamu kilikuwa ni upendo na utunzaji kwa mwanadamu. Tangu wakati ule binadamu alipopotoka hadi katika siku za mwisho za sasa, ingawaje Mungu anayo tabia ya haki, upendo na utunzaji Wake unabakia vilevile, haubadiliki. Hii inaonyesha kwamba kiini cha upendo wa Mungu, kuanzia uumbaji hadi sasa, licha ya kama binadamu amepotoka, haubadiliki.) (Leo niliona kwamba kiini cha Mungu hakitabadilika kutokana na mabadiliko ya muda au mahali pa kazi Yake. Niliona pia kwamba, haijalishi kama Mungu anauumba ulimwengu au anauangamiza baada ya binadamu kupotoka, kila kitu Anachofanya kina maana na kinayo tabia Yake. Hivyo basi niliona kwamba upendo wa Mungu hauna kikomo na haupimiki, niliona pia, kama vile ambavyo wale kaka na dada wengine, utunzaji na rehema ya Mungu kwa mwanadamu wakati Alipouangamiza ulimwengu.) (Haya ni mambo kwa hakika sikuyajua kuhusu hapo awali. Baada ya kusikiliza leo, nahisi kwamba Mungu ni wa ajabu kwa kweli, wa kuaminika kwa kweli, anayestahili kusadikiwa, na kwamba kwa kweli Yupo. Ninaweza kutambua kwa dhati ndani ya moyo wangu kwamba tabia ya Mungu na upendo wa Mungu kwa kweli ni vitu vinavyoshikika. Hii ndiyo hisia niliyo nayo baada ya kusikiliza leo.) Safi kabisa! Yaonekana nyote mmechukua kile mlichosikia na kukitia moyoni.

Je, mmetambua ukweli fulani kutoka mistari yote ya Biblia, zikiwemo hadithi zote za Biblia tulizowasiliana leo? Je, Mungu amewahi kutumia lugha Yake mwenyewe ili kuelezea fikira Zake binafsi au kuelezea upendo na utunzaji Wake kwa binadamu? Kunayo rekodi ya Yeye kutumia lugha ya kawaida kutaja ni kiasi kipi ambacho Anajali na Anapenda mwanadamu? La! Je, si hayo ni kweli? Kuna wengi sana miongoni mwenu ambao wamesoma Biblia au vitabu vingine mbali na Biblia. Je, yupo yeyote kati yenu aliyeyaona maneno kama hayo? Jibu bila shaka ni la! Yaani, kwenye rekodi za Biblia, yakiwemo maneno ya Mungu au urekodi wa kazi Yake, Mungu

hajawahi katika enzi yoyote au kipindi chochote kile kutumia mbinu Zake mwenyewe kufafanua hisia Zake au kuelezea upendo na utunzaji Wake kwa mwanadamu wala Mungu hajawahi kutumia matamshi au vitendo kufikisha hisia na mawazo Yake—Je, si hiyo ni ukweli? Kwa nini Ninasema hivyo? Kwa nini lazima Nitaje hii? Ni kwa sababu hii pia inayo uzuri wa Mungu na tabia Yake.

Mungu aliwaumba wanadamu; licha ya kama wamepotoka au kama wanamfuata Yeye, Mungu hushughulikia binadamu kama wapendwa Wake wanaothaminiwa zaidi—au kama vile binadamu wangesema, watu walio wapenzi Wake sana—na wala si kama vikaragosi Wake. Ingawaje Mungu anasema Yeye ndiye muumba na kwamba binadamu ni uumbaji Wake, hali ambayo inaweza kuonekana ni kana kwamba kuna tofauti kiasi katika mpangilio wa cheo, uhalisia ni kwamba kila kitu ambacho Mungu amefanya kwa mwanadamu kinazidi kabisa uhusiano wa asili hii. Mungu anampenda mwanadamu, anamtunza mwanadamu, na anaonyesha kwamba anamjali mwanadamu, pamoja na kumkimu mwanadamu bila kuacha na bila ya kusita. Kamwe hahisi katika moyo Wake kwamba hii ni kazi ya ziada au ni kitu kinachostahili sifa nyingi. Wala Hahisi kwamba kuokoa binadamu, kuwatosheleza, na kuwapatia kila kitu, ni kutoa mchango mkuu kwa binadamu. Anamkimu tu mwanadamu kimyakimya na kwa unyamavu, kwa njia Yake mwenyewe na kupitia kwa kiini Chake na kile Anacho na alichio. Haijalishi ni toleo kiasi kipi na ni msaada kiasi kipi ambao wanadamu wanapokea kutoka kwa Yeye, Mungu siku zote hajawahi kufikiri kuhusu au kujaribu kutaka sifa yoyote. Hii inaamuliwa na kiini cha Mungu, na pia hasa ni maonyesho ya kweli pia ya tabia ya Mungu. Na ndio maana, haijalishi kama iko kwa Biblia au kitabu chochote kingine, hatujawahi kumpata Mungu akionyesha fikira Zake, na hatujawahi kumpata Mungu akifafanua au akitangazia wanadamu ni kwa nini Anafanya mambo haya, au ni kwa nini Anamjali sana mwanadamu, ili kumfanya mwanadamu kumshukuru Yeye au kumsifu Yeye. Hata wakati Amejeruhiwa, wakati moyo Wake umo katika maumivu makali, Hajawahi kusahau jukumu Lake kwa mwanadamu au wasiwasi Wake kwa mwanadamu, huku haya yote yakiendelea, Anavumilia madhara na maumivu akiwa pekee katika ukimya. Kinyume cha mambo ni kwamba, Mungu anaendelea kumkimu mwanadamu kama Anavyofanya siku zote. Ingawaje mwanadamu mara nyingi humsifia Mungu au huwa na ushuhuda Kwake, hakuna kati ya tabia hii ambayo imedaiwa na Mungu. Hii ni kwa sababu Mungu hajawahi kunuia mambo yoyote mazuri Anayomfanyia binadamu yeye pia naye kumfanyia vivyo hivyo kama ishara ya shukrani au ili iweze kuonekana kwamba anafanyiwa mazuri aliyofanya. Kwa mkono mwingine, wale wanaomcha Mungu na kujiepusha na maovu, wale wanaomfuata Mungu kwa kweli, wanaomsikiliza Yeye, na walio waaminifu Kwake yeye, na wale wanaomtii Yeye—hawa ndio watu ambao mara nyingi watapokea baraka za Mungu, na Mungu atawakabidhi baraka hizo bila kusita. Isitoshe, baraka ambazo watu hupokea kutoka kwa Mungu mara nyingi zinazidi

kufikiria kwao na pia zinazidi kitu chochote ambacho binadamu wanaweza kubadilishana na yale waliyofanya au gharama waliyolipia. Wakati mwanadamu anafurahia baraka za Mungu, Je, yupo yeyote anayejali ni nini Mungu anafanya? Je, yupo yeyote anayeonyesha wasiwasi wowote kuhusu vile ambavyo Mungu anahisi? Je, yupo yeyote anayethamini maumivu ya Mungu? Jibu la uhakika la maswali haya ni: La! Je, mwanadamu yeyote, akiwemo Nuhu, anaweza kuthamini yale maumivu ambayo Mungu alikuwa akihisi wakati huo? Je, mtu yeyote anaweza kufahamu ni kwa nini Mungu alianzisha agano kama hilo? Hakuna anayeweza! Mwanadamu hathamini maumivu ya Mungu si kwa sababu hawezi kuelewa maumivu ya Mungu, na si kwa sababu ya nafasi iliyopo kati ya Mungu na mwanadamu au tofauti kati ya hadhi yao; badala yake, ni kwa sababu mwanadamu hata hajali kuhusu hisia zozote za Mungu. Mwanadamu anafikiria Mungu yuko huru—Mungu hahitaji watu wa kujali kuhusu Yeye, kumwelewa au kumwonyesha namna anavyomfikiria. Mungu ni Mungu, hivyo Hana maumivu, hana hisia; Hatakasirika, Hahisi huzuni, hata Halii. Mungu ni Mungu, hivyo Hahitaji maonyesho yoyote ya kihisia na Hahitaji faraja yoyote ya kihisia. Kama Hahitaji mambo haya katika hali fulani, basi Atatatua mwenyewe na Hatahitaji usaidizi wowote kutoka kwa mwanadamu. Lakini kinyume chake ni kuwa, ni wale binadamu wanyonge, wanaohitaji tulizo, toshelezo, himizo la Mungu na hata pia kwake Yeye kuweza kutuliza hisia zao wakati wowote mahali popote. Fikira kama hiyo inajificha ndani kabisa ya mioyo ya mwanadamu: Binadamu ndiye mnyonge; wanahitaji Mungu ili awatunze kwa kila njia, wanastahili utunzaji wote wanaopokea kutoka kwa Mungu, na wanafaa kudai kutoka kwa Mungu chochote kile wanachohisi kinafaa kuwa ni chao. Mungu ndiye mwenye Nguvu; Anacho kila kitu, na Anahitaji kuwa mlezi wa mwanadamu na Anayetoa baraka. Kwa sababu Yeye tayari ni Mungu, Yeye Mwenyezi na Hahitaji katu chochote kutoka kwa mwanadamu.

Kwa vile binadamu hatilii maanani ufunuo wowote wa Mungu, hajawahi kuhisi huzuni, maumivu au furaha ya Mungu. Lakini kinyume chake ni kwamba, Mungu anajua maonyesho yote ya binadamu kama vile anavyojua sehemu ya kiganja cha mkono Wake. Mungu hutosheleza mahitaji ya kila mtu siku zote na pahali pote, akiangalia fikira zinazobadilika za kila mmoja na hivyo basi kuwatuliza na kuwahimiza, na kuwaongoza na kuwaangazia. Kuhusu mambo yote ambayo Mungu amemfanyia mwanadamu, na gharama zote Alizolipia kwa sababu yao, watu wanaweza kupata kifungu kutoka kwa Biblia au kutoka kwa chochote ambacho Mungu amesema mpaka sasa kinachoelezea waziwazi kwamba Mungu atadai kitu kutoka kwa binadamu? La! Kinyume cha mambo, haijalishi ni vipi watu wanapuuza kufikiria kwa Mungu, Bado Anawaongoza kwa marudio wanadamu, Anamkimu kwa kurudia mwanadamu na kumsaidia, kuwaruhusu kufuata njia za Mungu ili waweze kupokea hatima nzuri ambayo Amewatayarishia. Inapokuja kwa Mungu, kile Anacho na alichu, neema Yake, rehema Yake, na tuzo Zake zote,

zitakabidhiwa bila ya kusita kwa wale wanaompenda na kumfuata Yeye. Lakini hajawahi kufichua kwa mtu yeyote maumivu aliyopitia Yeye au hali ya akili Yake, na katu halalamiki kuhusu yeyote ambaye hamtilii Yeye maanani au hajui mapenzi Yake. Anavumilia tu haya yote kimyakimya, akisubiria siku ambayo mwanadamu ataweza kuelewa.

Kwa nini Nasema mambo haya hapa? Ni nini mnachoona kutoka kwa mambo haya Niliyosema? Kuna kitu katika kiini na tabia ya Mungu ambacho ndicho rahisi zaidi kupuuza, kitu ambacho kinamilikiwa tu na Mungu na wala si mtu yeyote, wakiwemo wale wengine wanafikiria kwamba ni watu wakubwa, watu wazuri, au Mungu wa kufikiria kwao. Kitu hiki ni nini? Ni kule kutokuwa na nafsi kwa Mungu. Tunapozungumzia kutokuwa na nafsi, unaweza kufikiria kwamba pia wewe huna nafsi, kwa sababu inapokuja kwa watoto wako, haujadiliani juu ya bei na wao na wewe ni mkarimu sana kwao, au unafikiria kwamba wewe huna nafsi sana inapokuja kwa wazazi wako. Haijalishi ni nini unafikiria, angaa unayo dhana ya neno “kutokuwa na nafsi” na unalifikiria kama neno zuri, na kwamba kuwa mtu asiye na nafsi ni jambo la kipekee. Wakati huna nafsi, unafikiri kuwa wewe ni mkubwa. Lakini hakuna mtu anayeweza kuona kutokuwa na nafsi kwa Mungu miongoni mwa viumbe wote, miongoni mwa watu, hafla, na vitu, na kupitia kazi ya Mungu. Kwa nini hali iko hivi? Kwa sababu binadamu ni mchoyo sana! Kwa nini Ninasema hivyo? Mwanadamu anaishi katika ulimwengu wa uyakinifu. Unaweza kumfuata Mungu, lakini huoni wala kushukuru namna ambavyo Mungu anakukimu, anavyokupenda na anavyoonyesha kwamba anakujali. Kwa hivyo unaona nini? Unaona watu wako wa ukoo wanaokupenda au kukupenda sana. Unayaona mambo ambayo ni ya manufaa kwa mwili wako, unajali kuhusu watu na vitu unavyopenda. Huku ndiko kutokuwa na nafsi kwa binadamu kunakodaiwa. Watu kama hao “wasiokuwa na nafsi” hata hivyo, huwa hawajali katu kuhusu Mungu anayewapa maisha. Kinyume na Mungu, kutokuwa na nafsi kwa binadamu kunakuwa cha nafsi na yenye uchoyo. Kutokuwa na nafsi ambako binadamu anasadiki katika ni ulio mtupu na usio halisi, uliotiwa madoa, usiolingana na Mungu, na usiohusika na Mungu. Kutokuwa na nafsi kwa binadamu ni kwa ajili yake, huku kutokuwa na nafsi kwa Mungu ni ufunuo wa kweli wa kiini Chake. Ndipo hasa kutokana na kujitolea nafsi kwa Mungu ndipo binadamu anapokea mfululizo usiosita wa ujazo kutoka kwake. Huenda msiathirike sana na mada hii Ninayozungumza kuhusu leo na unaweza kuwa tu unatikisa kichwa chako kwa kukubaliana nami, lakini wakati unapojaribu kufurahia moyo wa Mungu katika moyo wako, utaweza kwa kutojua kugundua: Miongoni mwa watu wote, masuala, na mambo unaweza kuhisi katika ulimwengu huu ni kutokuwa na nafsi tu kwa Mungu ambako ni kweli na dhabiti, kwa sababu ni upendo wa Mungu tu kwako ndio ambao hauna masharti na hauna madoa. Mbali na Mungu, kutokuwa na kile kinachodaiwa kutokuwa na nafsi wa mtu mwingine ni bandia, cha juujuu, kisicho na msingi; kina kusudio, nia fulani, kinatekeleza shughuli ya masikilizano, na hakiwezi

kupimwa kamwe. Mnaweza hata kusema kwamba ni ki chafu, na cha kudharauliwa. Je, mnakubali?

Ninajua hamjazoeana na mada hizi na mnahitaji muda kidogo ili ziweze kuingia ndani yenu kabla muweze kuelewa kwa kweli. Kwa kadri mnavyokuwa kwamba hamjazoeana na masuala na mada hizi, ndipo inapothibitisha zaidi kwamba mada hizi zinakosekana katika mioyo yenu. Kama Singetaja mada hizi, yupo yeyote kati yenu ambaye angeweza kujua kidogo kuzihusu? Nasadiki hamngewahi pata kuyajua. Hii ni ya hakika. Haijalishi ni kiasi kipi mnachoweza kufahamu au kuelewa, kwa ufupi, mada hizi Ninazozungumzia ndizo ambazo watu wanakosa sanasana na wanazofaa kujua kuhusu zaidi. Mada hizi ni muhimu kwa kila mmoja—ni zenye thamani na ndiyo maisha, na ni mambo ambayo lazima mmiliki vizuri kwa safari ijayo. Bila ya maneno haya kama mwongozo, bila ya uelewa wako wa tabia ya Mungu na kiini, siku zote utabakia na alama ya kiulizo inapokuja kwa Mungu. Unawezaje kusadiki kwa Mungu kwa njia bora kama hata humwelewi Yeye? Hujui chochote kuhusu hisia Zake, mapenzi Yake, hali ya akili Yake, kile Anachofikiria, nini kinachomfanya Yeye kuwa na huzuni, na nini kinachomfanya Yeye kuwa na furaha, hivyo unawezaje kuweka moyo wa Mungu katika fikira?

Kila wakati Mungu anapokuwa amekasirika, Anakumbana na mwanadamu ambaye hamtilii maanani kamwe, mwanadamu anayemfuata Yeye na anayedai kumpenda Yeye lakini anapuuza kabisa hisia Zake. Moyo Wake utakosaje kuumia? Katika kazi ya usimamizi ya Mungu, Anaitekeleza kwa dhati kazi Yake na Anaongea na kila mmoja Anawatazama bila kizuizi chochote au kujificha, lakini kinyume chake ni kuwa, kila mtu anayemfuata Yeye anateganishwa na Yeye, na hakuna aliye radhi kujishughulisha na kuwa karibu na Yeye, kuelewa moyo Wake, au kutilia maanani hisia Zake. Hata wale wanaotaka kuwa wandani wa Mungu hawataki kuwa karibu na Yeye, kutilia maanani moyo Wake, au kujaribu kumwelewa Yeye. Wakati Mungu anashangilia na ana furaha, hakuna yeyote yule wa kushiriki katika furaha hiyo na Yeye. Wakati Mungu anakosa kueleweka na watu, hakuna mtu wa kutuliza moyo Wake ulio na majeraha. Wakati moyo Wake unaumia, hakuna hata mtu mmoja aliye radhi kumsikiliza Yeye na kuwa mwandani Wake. Katika hii maelfu ya miaka ya usimamizi wa kazi ya Mungu, hakuna mtu anayeelewa hisia za Mungu, hakuna hata mtu anayefahamu au kutambua hisia Zake, tupilia mbali hata yeyote ambaye angesimama kando ya Mungu ili kushiriki katika furaha na huzuni Zake. Mungu ni mpweke. Yeye ni pweke! Mungu ni mpweke si tu kwa sababu wanadamu waliopotoka wanampinga Yeye, lakini zaidi kwa sababu wale wanaofuatilia kuwa wa kiroho, wale wanaotafuta kumjua Mungu na kumwelewa Yeye, na hata wale walio radhi kujitolea maisha yao yote kwake Yeye, pia hawajui fikira Zake, na hawaelewi tabia Yake na hisia Zake.

Mwishoni mwa hadithi ya Nuhu, tunaona kwamba Mungu alitumia mbinu isiyo ya kawaida kuelezea hisia Zake wakati huo. Mbinu hii ni maalumu sana, na ni kuweka agano na binadamu. Ni mbinu inayotangaza mwisho wa matumizi ya gharika na Mungu katika kuangamiza ulimwengu. Kutoka nje, kuweka agano kunaonekana kuwa jambo lililo la kawaida sana. Si jambo lolote zaidi ya kutumia maneno kufunga wahusika ili wasitende vitendo vitakavyokiuka agano, ili kusaidia kutimiza kusudio la kulinda maslahi ya pande zote mbili. Kwa umbo, ni jambo la kawaida sana, lakini kutoka kwa motisha zilizopo na maana ya Mungu kufanya kitu hiki, ni ufunuo wa kweli wa tabia ya Mungu na hali Yake ya akili. Endapo utayaweka maneno haya kando na kuyapuuza, kama Sitawahi kukuambia ukweli wa mambo, basi binadamu hawatawahi kwa hakika kujua kufikiria kwa Mungu. Pengine katika kufikiria kwako Mungu alikuwa akitabasamu wakati alipofanya agano hili, au pengine maonyesho Yake yalikuwa mazito, lakini haijalishi ni watu wanavyofikiria Mungu alikuwa na maonyesho gani ya kawaida kabisa, hakuna ambaye angeweza kuuona moyo wa Mungu au maumivu Yake, na hata upweke Wake. Hakuna mtu anayeweza kumfanya Mungu kumwamini au anayestahili kuaminiwa na Mungu, au kuwa mtu Anayeweza kueleza fikira Zake au kuwa mwandani Wake wa kuambia maumivu Yake. Ndiyo maana Mungu hakuwa na chaguo ila kufanya kitu kama hicho. Kwa juujuu, Mungu alifanya jambo rahisi la kuwaaga binadamu wale wa awali, kuhitimisha hali ya kale ilivyokuwa na kufikia hitimisho halisi katika kuangamiza Kwake kwa ulimwengu akitumia gharika. Hata hivyo, Mungu alikuwa ameyazika maumivu kutoka muda huu ndani kabisa ya moyo Wake. Kwa wakati ambao Mungu hakuwa na yeyote wa kuita mwandani, aliunda agano na wanadamu, akiwaambia kwamba asingeuangamiza ulimwengu kwa gharika tena. Wakati upinde wa mvua unapojitokeza ni kukumbusha watu kwamba, kitu kama hicho kiliwahi kufanyika, kuwapa onyo watu dhidi ya kufanya maovu. Hata katika hali hiyo ya maumivu, Mungu hakusahau kuwahusu wanadamu na bado akaonyesha kujali kwingi sana kwao. Je, huu si upendo na kutokuwa na nafsi kwa Mungu? Lakini nao watu wanafikiria nini wakati wanapoteseka? Kwani huu si wakati ambao wanamhitaji Mungu zaidi? Katika nyakati kama hizi, siku zote watu humkokota Mungu katika mambo yao ili Mungu aweze kuwapa tulizo. Haijalishi ni lini, Mungu hatawahi kuwavunja moyo watu wake, na siku zote Atawaruhusu watu kutoka katika changamoto zao na kuishi katika mwangaza. Ingawaje Mungu anawakimu wanadamu, ndani wa moyo wa binadamu, Mungu si chochote wala lolote ila tembe ya kumhakikishia tu mambo, dawa ya tulizo. Wakati Mungu anateseka, wakati moyo Wake una majeraha, kuwa na kiumbe aliyeumba au mtu yeyote wa kuwa mwandani wake au wa kumtuliza Yeye kwa kweli kwake Mungu ni tamanio tu la kibadhirifu asiloweza kutegemea. Siku zote binadamu hatilii maanani hisia za Mungu, hivyo Mungu siku zote haulizii wala hatarajii kuwa kuna mtu anayeweza kumtuliza Yeye. Anatumia mbinu Zake mwenyewe kueleza hali Yake. Watu hawafikirii kwamba ni jambo kubwa kwa Mungu kupitia mateso fulani, lakini unapojaribu tu

kuelewa Mungu kwa kweli, unapoweza kushukuru kwa dhiti, nia nzuri za Mungu katika kila kitu anachofanya, ndipo unapoweza kuhisi ukubwa wa Mungu na kutokuwa na nafsi kwake. Ingawaje Mungu aliunda agano na wanadamu kutumia upinde wa mvua, hakuwahi kuambia yeyote kwa nini alifanya hivi, kwa nini alianzisha agano hili, kumaanisha hakuwahi kuambia mtu fikira Zake halisi. Hii ni kwa sababu hakuna mtu anayeweza kufahamu kina cha upendo ambao Mungu anao kwa wanadamu Aliowaumba kwa mikono Yake mwenyewe, na hakuna pia mtu anayeweza kutambua ni kiasi kipi cha maumivu moyo Wake uliteseka wakati Alipoangamiza binadamu. Hivyo basi, hata kama Angeambia watu namna Anavyohisi, hawawezi kumwamini. Licha ya kuwa katika maumivu, angali Anaendelea na hatua inayofuata ya kazi Yake. Siku zote Mungu Anautoa upande wake bora zaidi na mambo bora zaidi kwa wanadamu huku yeye Mwenyewe Akistahimili kimyakimya mateso yote. Mungu kamwe hafichui mateso haya. Badala yake, Anayavumilia na kusubiri kwa kimya. Ustahimilivu wa Mungu si wa kimya tu, usio na hisia, au usio na suluhu, wala si ishara ya unyonge. Ni kwamba upendo na kiini cha Mungu siku zote yamekuwa bila nafsi. Huu ni ufunuo wa kiasili wa kiini na tabia Yake na maonyesho halisi wa utambulisho wa Mungu kama Muumba wa kweli.

Baada ya kusema hayo, wengine wanaweza kufasili vibaya kile Ninachomaanisha. “Je kufafanua hisia za Mungu kwa maelezo kama hayo, kwa hali ya hisia nyingi sana, inanuia kuwafanya watu kuhisi masikitiko kwa Mungu?” Je, hayo ndiyo madhumuni hapa? (La!) Kusudio la pekee la Mimi kusema maneno haya ni kuwafanya kujua Mungu kwa njia bora zaidi, kuelewa kila sehemu Yake, kuelewa hisia Zake, kutambua kiini na tabia ya Mungu, kwa uthabiti na kwa kidogo kidogo, iliyoelezewa kupitia kwa kazi Yake, kinyume na vile inavyotumiwa kupitia kwa maneno matupu ya binadamu, barua na mafundisho yao ya kidini, au kufikiria kwao. Hivi ni kusema, Mungu na kiini cha Mungu kwa kweli vipo—si tu uchoraji, havijafikiriwa, havijajengwa na binadamu, na bila shaka havijabuniwa na wao. Je, mnatambua hii sasa? Kama mnaitambua, basi maneno Yangu leo yametimiza shabaha yao.

Tulijadili mada tatu leo. Nina imani kwamba kila mmoja amepata pakubwa kutoka katika ushirika wetu juu ya mada hizi tatu. Ninaweza kusema kwa hakika kwamba, kupitia kwa mada hizi tatu, fikira za Mungu Nilizofafanua au kiini cha Mungu na tabia Nilizotaja vyote vimebadili mawazona ufahamu wa watu kuhusu Mungu, hata kubadili imani za kila mmoja kwa Mungu, na zaidi, kubadili picha ya Mungu inayopendwa na kila mmoja katika mioyo yao. Haijalishi ni nini, Natumai kwamba kile mmejifunza kuhusu tabia ya Mungu katika sehemu hizi tatu za Biblia ni cha manufaa kwenu, na Natumai kwamba baada ya nyinyi kurudi mtajaribu kukitafakari zaidi. Kikao cha leo kinahitimishwa hapa. Kwaheri!

Novemba 4, 2013

Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe II

Katika mkutano wetu wa mwisho tuliweza kuzungumzia mada muhimu sana. Je, mnakumbuka mada hiyo ilikuwa kuhusu nini? Hebu Niirudie. Mada ya ushirika wetu wa mwisho ilikuwa: Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe. Je, mada hii ni muhimu kwenu? Ni sehemu gani katika mada hii ni muhimu kwenu? Kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, au Mungu Mwenyewe? Ni sehemu ipi inawavutia zaidi? Ni sehemu ipi mnayotaka kusikiliza kuhusu zaidi? Najua ni vigumu kwenu ninyi kulijibu swali hilo, kwa sababu tabia ya Mungu inaweza kuonekana katika kila kipengele cha kazi Yake, na tabia Yake inafichuliwa katika kazi Yake siku zote na pahali pote, na, kutokana na hayo, inawakilisha Mungu Mwenyewe; kwenye mpango wa usimamizi wa ujumla wa Mungu, kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe vyote hivi haviwezi kutenganishwa.

Maudhui ya ushirika wetu wa mwisho kuhusu kazi ya Mungu yaliweza kuangazia mambo yaliyofanyika kitambo kwenye Biblia. Maudhui hayo yote yalikuwa hadithi kuhusu binadamu na Mungu, na yalimfanyikia binadamu na wakati huohuo yakahusisha kushiriki na maonyesho ya Mungu, hivyo basi hadithi hizi zinashikilia thamani na umuhimu mkubwa katika kujua Mungu. Baada tu ya kuumba binadamu, Mungu Alianza kujihusisha na binadamu na kuzungumza na binadamu, na tabia yake ikaanza kuonyeshwa kwa binadamu. Kwa maneno mengine, tangu Mungu alipojihusisha kwanza na wanadamu, Alianza kuweka wazi kwa mwanadamu, bila kusita, kiini Chake halisi na kile Anacho na alichio. Licha ya kama watu wa awali au watu wa leo wanaweza kuona au kuelewa kiini hicho, kwa ufupi Mungu anamzungumzia mwanadamu na kufanya kazi miongoni mwa binadamu, Akifichua tabia Yake na Akionyesha kiini Chake—jambo ambalo ni ukweli, na lisilopingika na mtu yeyote. Hii inamaanisha pia kwamba tabia ya Mungu, kiini cha Mungu, na kile Anacho na alichio vyote vinatolewa daima na kufichuliwa huku naye Akifanya kazi na kujihusisha na binadamu. Hajawahi kusetiri au kumfichia binadamu chochote, lakini badala yake anatangaza kwa umma na kuachilia tabia Yake binafsi bila ya kuficha chochote. Hivyo basi, Mungu anatumai kwamba binadamu anaweza kumjua Yeye na kuelewa tabia Yake na kiini chake. Hapendi binadamu kuchukulia tabia Yake na kiini Chake kuwa mafumbo ya milele, wala Hataki wanadamu kumchukulia Mungu kama fumbo lisiloweza kutatuliwa. Mpaka tu pale ambapo wanadamu watakapomjua Mungu ndipo binadamu atakapojua njia ya kufuata na kuweza kuukubali mwongozo wa Mungu, na wanadamu tu kama hawa ndio wanaoweza kuishi kwa kweli katika utawala wa Mungu, na kuishi katika mwangaza, na kuishi katikati ya baraka za Mungu.

Maneno na tabia iliyowasilishwa mbele na kufichuliwa na Mungu inawakilisha mapenzi Yake, na pia inawakilisha kiini Chake halisi. Wakati Mungu anapojihusisha na binadamu,

haijalishi ni nini Anachosema au kufanya, au tabia gani Anayofichua, na haijalishi ni nini binadamu anaona kuhusu kiini cha Mungu na kile Anacho na alichu, vyote vinawasilisha mapenzi ya Mungu kwa binadamu. Licha ya kiwango ambacho binadamu anaweza kutambua, kufahamu, au kuelewa, vyote hivi vinawakilisha mapenzi ya Mungu—mapenzi ya Mungu kwa binadamu. Hili ni bila shaka! Mapenzi ya Mungu kwa binadamu ni vile Anavyohitaji watu kuwa, kile Anachohitaji wao kufanya, namna Anavyohitaji wao kuishi, na vile Anavyowahitaji kuweza kukamilisha kutimia kwa mapenzi ya Mungu. Je, mambo haya hayawezi kutenganishwa na kiini cha Mungu? Kwa maneno mengine, Mungu huwasilisha mbele tabia Yake na chote Alichu nacho na alichu wakati huohuo Akimtolea madai binadamu. Hakuna uongo, hakuna kusingizia, hakuna ufichaji, na wala hakuna kupiga chuku. Ilhali kwa nini binadamu hawezi kujua na kwa nini hajawahi kuweza kutambua waziwazi tabia ya Mungu? Na kwa nini hajawahi kutambua mapenzi ya Mungu? Kile ambacho kimefichuliwa na kuwasilishwa mbele na Mungu ndicho kile Mungu anacho Mwenyewe na maana yake, na kinaonyesha kila kipengele cha tabia Yake ya kweli—hivyo kwa nini binadamu hawezi kuona? Kwa nini binadamu hana uwezo wa kuwa na maarifa ya kina? Kunayo sababu muhimu ya haya. Na sababu yenyewe ni ipi? Tangu wakati wa uumbaji, binadamu hajawahi kumchukulia Mungu kama Mungu. Kwenye nyakati zile za mwanzo kabisa, haikujalisha ni nini Mungu alifanya kuhusiana na binadamu, yule binadamu ambaye ndiye tu alikuwa ameumbwa, binadamu alimchukulia yeye kuwa mwandani wake tu na wala si zaidi ya hapo, kama mtu wa kutegemewa, na hakuwa na maarifa yoyote wala uelewa wa Mungu. Hivi ni kusema, hakujua kwamba kile kilichowasilishwa mbele na Kiumbe huyu—Kiumbe huyu ambaye yeye alitegemea na kumwona kuwa mwandani wake—alikuwa kiini cha Mungu, na wala hakujua kwamba Kiumbe huyu ndiye anayetawala viumbe wote. Nikisema kwa urahisi, watu wa wakati huo hawakuwa na maarifa hata kidogo kumhusu Mungu. Hawakujua kwamba mbingu na nchi na mambo yote yalikuwa yameumbwa na Yeye na wala hawakujua ni wapi Alipotokea, na, zaidi hawakujua Yeye Alikuwa nani. Bila shaka, wakati huo Mungu hakumhitaji binadamu kumjua Yeye au kumfahamu Yeye au kuelewa kila kitu Alichofanya, au kufahamishwa kuhusu mapenzi Yake, kwani hizi zilikuwa nyakati za mapema zaidi baada ya uumbwaji wa wanadamu. Wakati Mungu alipoanza matayarisho ya kazi ya Enzi ya Sheria, Mungu alifanya mambo fulani kwa binadamu na pia Akaanza kutolea binadamu madai fulani, Akimwambia namna ya kutolea Mungu sadaka na namna ya kumwabudu. Ni wakati huo ndipo binadamu alipopata mawazo machache mepesi kuhusu Mungu, ni hapo tu ndipo alipojua tofauti kati ya binadamu na Mungu na kwamba Mungu Ndiye aliyewaumba wanadamu. Wakati binadamu alipojua kwamba Mungu alikuwa Mungu na binadamu alikuwa binadamu kukawa umbali fulani kati ya Yeye na Mungu, bado Mungu hakuhitaji kwamba binadamu awe na maarifa makuu au uelewa wa kina kumhusu Yeye. Hivyo basi, Mungu anayatoa mahitaji tofauti kwa binadamu kutokana na awamu na hali za kazi Yake. Mnaona nini katika haya? Ni kipengele

kipi cha tabia ya Mungu unayoitambua? Je, Mungu ni wa kweli? Yale mahitaji ambayo Mungu anampa binadamu yanastahili? Kwenye nyakati za mapema kabisa kufuatia uumbaji wa wanadamu na Mungu, wakati ambao Mungu alikuwa bado hajatekeleza kazi ya ushindi na utimilifu wa binadamu, na Alikuwa hata bado hajaongea yale maneno mengi sana kwake, Alihitaji kidogo sana kutoka kwa binadamu. Licha ya kile ambacho binadamu alifanya na namna alivyotenda—hata kama alifanya mambo fulani yaliyomkosea Mungu—Mungu alimsamehe hayo yote, na akayapuuza. Hii ni kwa sababu Mungu Alijua kile Alichokuwa Amempa binadamu na kile kilichokuwa ndani ya binadamu, na basi Alijua kiwango cha mahitaji ambayo anafaa kudai kutoka kwa binadamu. Ingawaje kiwango cha mahitaji Yake kilikuwa cha chini sana wakati huo, hii haimaanishi kwamba tabia Yake haikuwa kuu, au kwamba hekima na uweza Wake yalikuwa si yoyote ila maneno matupu. Kwa binadamu, kunayo njia moja tu ya kujua tabia ya Mungu na Mungu Mwenyewe: kwa kufuata hatua za kazi ya usimamizi ya Mungu na wokovu wa wanadamu, na kuyakubali maneno ambayo Mungu anaongea akiyaelekeza kwa wanadamu. Kujua kile Mungu anacho na alichu, na kujua tabia ya Mungu, bado binadamu angemuuliza Mungu kumwonyesha nafsi Yake halisi? Binadamu hatafanya hivyo, na hathubutu kufanya hivyo, kwa kuweza kuifahamu tabia ya Mungu na kile Anacho na alichu, tayari binadamu atakuwa amemwona Mungu Mwenyewe wa kweli, na atakuwa tayari ameona nafsi Yake halisi. Haya ndiyo matokeo yasiyoepukika.

Kazi na mpango wa Mungu ulipokuwa ukiendelea mbele bila kusia, na baada ya Mungu kuanzisha agano la upinde wa mvua na binadamu kama ishara kwamba Hangewahi tena kuuangamiza ulimwengu kwa kutumia gharika, Mungu alikuwa na tamanio lililokuwa likiongezeka na kumsukuma kuwapata wale ambao wangeweza kuwa katika akili moja na Yeye. Hivyo, pia, Alikuwa na tamanio la haraka zaidi la kupata wale waliokuwa na uwezo wa kufanya mapenzi Yake duniani, na, isitoshe, kupata kundi la watu ambao wangeweza kuwa huru dhidi ya nguvu za giza, na kutoweza kuwa watumwa wa Shetani, na kuweza kuwa na ushuhuda kwake Yeye duniani. Kupata kundi la watu kama hawa kulikuwa ni tamanio la Mungu kwa muda mrefu, Alichokuwa akisubiria tangu wakati wa uumbaji. Hivyo basi, licha ya matumizi ya gharika na Mungu ili kuuangamiza ulimwengu, au agano Lake na binadamu, mapenzi ya Mungu, hali yake ya akili, mpango, na matumaini yote yalibakia yaleyale. Kile Alichotaka kufanya, ambacho Alikuwa ametamani kwa muda mrefu kabla ya uumbaji, kilikuwa kupata wale walio miongoni mwa wanadamu ambao Alitamani kuwapata—Kupata watu wa kundi hili ambao walioweza kufahamu na kujua tabia Yake, na kuyaelewa mapenzi Yake, kundi ambalo lingeweza kumwabudu Yeye. Watu kwenye kundi kama hili wanaweza kweli kuwa na ushuhuda kwake, na wao ndio, yaweza kusemekana, wasiri Wake.

Leo, hebu tuendeleo kuzifuata nyayo za Mungu na kufuata nyayo za kazi Yake, ili tuweze

kufichua fikira na mawazo ya Mungu, na vipengele vyote mbali mbali vinayomhusu Mungu, vyote ambavyo “vimefungwa kabisa” kwa muda mrefu sana. Kupitia mambo haya tutajua hatimaye tabia ya Mungu, kukielewa kiini cha Mungu, tutamruhusu Mungu kuingia kwenye mioyo yetu, na kila mmoja wetu ataweza kukaribia Mungu kwa utaratibu, na kupunguza umbali wetu na Mungu.

Sehemu ya kile tulichozungumzia wakati wa mwisho ilihusiana na kwa nini Mungu alianzisha agano na binadamu. Wakati huu, tutakuwa na ushirika kuhusu vifungo vya maandiko vilivyo hapa chini. Hebu tuanze kwa kuyasoma maandiko.

A. Ibrahimu

1. Mungu Amwahidi Ibrahimu Mwana

Mwa 17:15-17 Naye Mungu akasema kwake Ibrahimu, na kuhusu Sarai mke wako, hutamwita kwa jina lake la Sarai, kwa maana sara ndilo litakuwa jina lake. Na mimi nitambariki yeye, na pia nitakupa mwana kutoka kwake: ndiyo, nitambariki yeye, na yeye atakuwa mama yao mataifa; wafalme wa watu watatoka kwa yeye. Kisha Ibrahimu akaanguka chini kifudufudi, na kucheka, na akasema moyoni, Je, mtoto atazaliwa kwa mtu mwenye umri wa miaka mia moja? naye Sara, aliye na umri wa miaka tisini, atazaa?

Mwa 17:21-22 Lakini nitaliimarisha agano Langu na Isaka, ambaye Sara atakuzalia wewe wakati kama huu mwaka ujao. Naye Akakoma kuzungumza na yeye, na Mungu akapanda juu kutoka kwa Ibrahimu.

2. Ibrahimu Amtoa Isaka

Mwa 22:2-3 Naye Akasema, Umchukue mwana wako sasa, mwana wako wa pekee Isaka, unayempenda, na uende hadi nchi ya Moria; na huko umtoe kwa sadaka ya kuteketezwa juu ya mojawapo ya milima ambayo nitakuambia. Naye Ibrahimu akaamka asubuhi mapema, na kuweka tandiko kwa punda wake, akawachukua vijana wake wawili pamoja naye, naye Isaka mwana wake, na akapasua kuni kwa sababu ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, na akaondoka, na kuenda pahali ambapo alikuwa ameambiwa na Mungu.

Mwa 22:9-10 Na wakafika pahali hapo ambapo Mungu alikuwa amemwambia; naye Ibrahimu akajenga madhabahu hapo, na kuziweka kuni kwa mpango, na kumfunga Isaka mwana wake, naye akamlaza juu ya madhabahu kwa zile kuni. Na Ibrahimu akanyosha mbele mkono wake, na kukichukua kisu ili amchinje mwana wake.

Hakuna Awezaye Kuzuia Kazi Ambayo Mungu Anaamua Kufanya

Hivyo, muda mfupi uliopita nyote mmesikia hadithi ya Ibrahimu. Alichaguliwa na Mungu baada ya gharika kuuangamiza ulimwengu, jina lake lilikuwa Ibrahimu, na alipokuwa na miaka mia moja, na mke wake Sara akiwa na umri wa miaka tisini, ahadi ya Mungu ilimjia. Mungu alimwahidi nini? Mungu alimwahidi kile ambacho kinarejelewa katika Maandiko: “Na mimi nitambariki yeye, na pia nitakupa mwana kutoka kwake.” Ni maelezo yapi yalitangulia ahadi ya Mungu ya kumpa mtoto? Maandiko yanaelezea yafuatayo: “Kisha Ibrahimu akaanguka chini kifudifudi, na kucheka, na akasema moyoni, Je, mtoto atazaliwa kwa mtu mwenye umri wa miaka mia moja? naye Sara, aliye na umri wa miaka tisini, atazaa?” Kwa maneno mengine wanandoa hawa wazee walikuwa na umri mwingi sana wa kupata watoto. Naye Ibrahimu alifanya nini baada ya Mungu Kumwahidi? Aliuangukia uso wake akicheka, na kujiambia, “Je, mtoto atazaliwa kwa mtu mwenye umri wa miaka mia moja?” Ibrahimu aliamini kwamba haikuwezekana—hivi alimaanisha kwamba alisadiki ahadi ya Mungu kwake haikuwa chochote ila mzaha. Kutoka mtazamo wa binadamu, ahadi isingeweza kutimizika na binadamu, na vilevile isingeweza kutimizika na Mungu na ilikuwa haiwezekani kwa Mungu. Pengine, kwa Ibrahimu, ahadi hii ilikuwa ya kuchekesha. Mungu alimuumba binadamu, lakini yaonekana kwamba hajui kwamba mtu aliyezeeka sana hawezi kupata watoto; Anafikiria kwamba Anaweza kuniruhusu kupata mtoto, Anasema kwamba atanipa mtoto—kwa kweli hilo haliwezekani! Na hivyo, Ibrahimu akaangukia uso wake na kucheka, akijifikiria yeye mwenyewe: Haiwezekani—Mungu anafanya mzaha na mimi, hili haliwezi kuwa kweli. Hakutilia maanani maneno yake Mungu. Hivyo, katika macho ya Mungu, Ibrahimu alikuwa binadamu wa aina gani? (Mwenye haki.) Ni wapi ulipojifunza kwamba alikuwa mwenye haki? Ninyi mnafikiria kwamba wale wote ambao Mungu anawaita ni wenye haki, na watimilifu, na watu wanaotembea na Mungu. Wewe unashikilia mafundisho ya dini! Lazima uone waziwazi kwamba wakati Mungu anapomfasili mtu, Hafanyi hivyo kiholela. Hapa, Mungu hakusema kwamba Ibrahimu alikuwa mwenye haki. Katika moyo Wake, Mungu anavyo viwango vya kupima kila mtu. Ingawaje Mungu hakusema ni mtu wa aina gani ambaye Ibrahimu alikuwa, kwa mujibu wa mwenendo wake, Ibrahimu alikuwa na imani ya aina gani kwake Mungu? Ilikuwa ya kidhahania kidogo? Au alikuwa mwenye imani kuu? La, hakuwa! Kicheko na fikira zake zilionyesha yeye alikuwa nani, hivyo imani yenu kwamba alikuwa mwenye haki ni ndoto ya kufikiria kwenu, ni matumizi yasiyo na mwelekeo ya mafundisho ya dini, usiopaswa. Je, Mungu alikiona kicheko cha Ibrahimu na maonyesho yake madogo, Alijua kuyahusu? Mungu alijua. Lakini Mungu angebadilisha kile Alichokuwa ameamua kufanya? La! Wakati Mungu alipopangilia na kuamua kwamba Angemchagua binadamu huyu, suala hilo lilikuwa tayari limekamilishwa. Si fikira za binadamu wala mwenendo wake ungemshawishi au kuhitilafiana na Mungu hata chembe; Mungu Asingebadilisha kiholela mpango Wake, wala Asingebadilisha au kuharibu mpango Wake kwa sababu ya mwenendo wa binadamu, hali ambayo ingekuwa ujinga. Nini, basi, kimeandikwa

katika Mwanzo 17:21-22? “Lakini nitaliimarisha agano langu na Isaka, ambaye Sara atakuzalia wewe wakati kama huu mwaka ujao. Naye akakoma kuzungumza na yeye, na Mungu akapanda juu kutoka kwa Ibrahimu.” Mungu hakutilia maanani hata chembe kile Ibrahimu alichofikiria au kusema. Na sababu ya kutotilia maanani Kwake ni gani? Kutotilia maanani kwake kulikuwa kwa sababu, wakati huo Mungu hakuhitaji kwamba mwanadamu awe mwenye imani kuu au kwamba aweze kuwa na maarifa makuu kuhusu Mungu, au, vilevile, aweze kuelewa kile kilichofanywa na kusemwa na Mungu. Hivyo, hakuhitaji kwamba binadamu aelewe kabisa kile Alichoamua kufanya, au watu Alioamua kuchagua, au kanuni za vitendo Vyake, kwani kimo cha binadamu hakikutosha tu. Wakati huo, Mungu alichukulia kile ambacho Ibrahimu alifanya na vyovyote alivyojiendesha yeye mwenyewe kuwa kawaida. Hakushutumu, au kukemea, lakini alisema tu: “Sara atakuzalia Isaka wakati huu uliopangwa mwaka ujao.” Kwa Mungu, baada Yake kuyatangaza maneno haya, suala hili hatimaye lilikuwa kweli hatua kwa hatua; katika macho ya Mungu, kile ambacho kilikuwa kikamilishwe na mpango Wake kilikuwa tayari kimetimizwa. Baada ya kuikamilisha mipangilio ya hayo, Mungu aliondoka. Kile binadamu hufanya au kufikiria, kile binadamu huelewa, mipango ya binadamu—hakuna chochote kati ya hivi vyote kinacho uhusiano wowote na Mungu. Kila kitu hufanyika kulingana na mpango wa Mungu, kikiendana na nyakati na awamu zilizowekwa na Mungu. Hivyo ndivyo kanuni ya kazi ya Mungu inavyoenda. Mungu haingilii kati chochote kile binadamu anafikiria au kujua, ilhali Haachi mpango Wake, wala kuacha kazi Yake kwa sababu binadamu hasadiki wala kuelewa. Kweli hizi hivyo basi zinakamilishwa kulingana na mpango na fikira za Mungu. Hivi ndivyo hasa tunavyoona kwenye Biblia: Mungu Alisababisha Isaka kuzaliwa wakati ule Aliokuwa amepanga. Je, kweli zinathibitisha kwamba tabia na mwenendo wa binadamu vilizuia kazi ya Mungu? Havikuzuia kazi ya Mungu! Je, imani ndogo ya binadamu kwa Mungu, na dhana zake na fikira kumhusu Mungu viliweza kuathiri kazi ya Mungu? La, havikuathiri! Hata kidogo! Mpango wa usimamizi wa Mungu hauathiriwi na binadamu, suala, au mazingira yoyote. Kila kitu Anachoamua kufanya kitakamilika na kukamilishwa kwa wakati na kulingana na mpango Wake, na kazi Yake haiwezi kutatizwa na binadamu yeyote. Mungu hupuuza vipengele fulani vya ujinga na kutojua kwa binadamu, na hata upinzani na dhana fulani za binadamu Kwake, Akifanya kazi ambayo lazima Afanye bila ya kujali. Hii ni tabia ya Mungu na ni onyesho la kudura Yake.

Kazi ya Usimamizi wa Mungu na Wokovu wa Wanadamu Yaanza na Ibrahimu Kumtoa Isaka

Baada ya kumpa mtoto Ibrahimu, maneno ambayo Mungu alikuwa ametamka kwa Ibrahimu yakawa yametimizwa. Hii haimaanishi kwamba mpango wa Mungu ulifikia mwisho hapa; kinyume cha mambo ni kwamba, mpango wa ajabu wa Mungu wa usimamizi na wokovu wa

wanadamu ndipo ulikuwa tu umeanza, na baraka Yake ya mwana kwa Ibrahimu ilikuwa tu ni utangulizi wa mpango wa usimamizi Wake kwa ujumla. Wakati huo, ni nani aliyejua kwamba vita vya Mungu na Shetani vilikuwa vimeanza kimya kimya wakati Ibrahimu alipomtoa Isaka?

Mungu Hajali Kama Binadamu Ni Mjinga—Anahitaji Tu Binadamu Awe Mkweli

Kisha, hebu tuangalie kile Mungu alimfanyia Ibrahimu. Ukiangalia Mwanzo 22:2, Mungu alimtolea Ibrahimu amri ifuatayo: “Umchukue mwana wako sasa, mwana wako wa pekee Isaka, unayempenda, na uende hadi nchi ya Moria; na huko umtoe kwa sadaka ya kuteketezwa juu ya mojawapo ya milima ambayo nitakuambia.” Maana ya Mungu ilikuwa wazi: Alikuwa akimwambia Ibrahimu amtoe mtoto wake wa pekee Isaka, ambaye alimpenda, kwa minajili ya sadaka ya kuteketezwa. Tukiiangalia amri ya Mungu leo, je ingali inakinzana na dhana za binadamu? Ndiyo! Kile alichokifanya Mungu wakati huo ni kinyume sana na dhana za binadamu na hakieleweki kwa binadamu. Katika dhana zao, watu husadiki yafuatayo: Wakati binadamu hakusadiki, na akafikiria ni jambo lisilowezezana, Mungu Alimpa mwana, na baada ya kupata mtoto, Mungu alimwomba amtoe mwana wake—haiwezekani! Mungu kwa hakika alinua kufanya nini? Kusudio halisi la Mungu lilikuwa nini? Alimpa Ibrahimu mtoto bila masharti yoyote, ilhali pia Alimwomba Ibrahimu aweze kutoa bila masharti. Maji yalikuwa yamezidi unga? Katika mtazamo wa mtu wa pembeni, hapa maji hayakuwa tu yamezidi unga lakini pia ilikuwa kwa kiasi fulani hali ya “kuunda tatizo pasipo na tatizo.” Lakini Ibrahimu mwenyewe hakusadiki kwamba Mungu alikuwa akihitaji mengi sana. Ingawaje alikuwa na wasiwasi fulani, na alimshuku kidogo Mungu, alikuwa tayari bado kumtoa mtoto wake. Wakati huu, ni nini unachoona ambacho kinathibitisha kuwa Ibrahimu alikuwa radhi kumtoa mtoto wake? Ni nini kinazungumzwa kwenye sentensi hizi? Maandishi asilia yanaelezea yafuatayo: “Naye Ibrahimu akaamka asubuhi mapema, na kuweka tandiko kwa punda wake, akawachukua vijana wake wawili pamoja naye, naye Isaka mwana wake, na akapasua kuni kwa sababu ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, na akaondoka, na kuenda pahali ambapo alikuwa ameambiwa na Mungu” (Mwa 22:3). “Na wakafika pahali hapo ambapo Mungu alikuwa amemwambia; naye Ibrahimu akajenga madhabahu hapo, na kuziweka kuni kwa mpango, na kumfunga Isaka mwana wake, naye akamlaza juu ya madhabahu kwa zile kuni. Na Ibrahimu akanyosha mbele mkono wake, na kukichukua kisu ili amchinje mwana wake” (Mwa 22:9-10). Wakati Ibrahimu alipounyosha mkono wake na kukichukua kisu ili kumwua mtoto wake, Mungu aliviona vitendo vyake? Naam aliviona. Mchakato wote—kuanzia mwanzo, wakati Mungu alipomwomba Ibrahimu kumtoa Isaka, hadi pale ambapo Ibrahimu alikiinua kisu chake ili kumwua mtoto wake—hilo lilionyesha Mungu moyo wa Ibrahimu, na haijalishi kuhusu ujinga wake wa awali, kutojua kwake, na kutomwelewa Mungu kwake, wakati huo moyo wa Ibrahimu kwa Mungu ulikuwa kweli, na wenye uaminifu, na kwa kweli alikuwa akienda kumrudisha Isaka, mtoto aliyepewa yeye na

Mungu, ili arudi kwa Mungu. Ndani yake, Mungu aliuona utiifu, utiifu uleule ambao Yeye Alitamani.

Kwa binadamu, Mungu hufanya mengi yasiyoeleweka na yaliyo ya ajabu. Wakati Mungu anapotaka kupangilia mtu, mpango huu mara nyingi unakinzana na dhana za binadamu, na huwa haueleweki kwa binadamu huyo, ilhali ni ukosefu wa mwafaka huu na kutofahamu ndiyo majaribio ya Mungu na mtihani wake kwa binadamu. Ibrahimu, huku haya yakiendelea, aliweza kuonyesha utiifu kwa Mungu uliokuwa ndani yake, jambo ambalo ndilo lililokuwa sharti muhimu zaidi la yeye kuweza kushibisha mahitaji ya Mungu. Hapo tu, wakati Ibrahimu alipoweza kutii mahitaji ya Mungu, alipomtoa Isaka ndipo Mungu Alipohisi kwa kweli utulivu na kukubaliwa na wanadamu—kwa Ibrahimu, ambaye Alikuwa amemchagua. Hapo tu ndipo Mungu alipokuwa na hakika kwamba mtu huyu Aliyekuwa amemchagua Yeye alikuwa kiongozi muhimu ambaye angetekeleza ahadi Yake na mpango Wake wa usimamizi wa baadaye. Ingawaje lilikuwa tu jaribio na mtihani, Mungu alihisi furaha, Alihisi upendo wa binadamu kwake Yeye, na Alihisi akiwa ametulizwa na binadamu kwa mara ya kwanza. Wakati huu ambao Ibrahimu alipokiinua kisu chake ili kumwua Isaka, Mungu alimsimamisha? Mungu hakumruhusu Ibrahimu kumpa Isaka, kwani Mungu hakuwa na nia yoyote ya kumtoa uhai Isaka. Hivyo, Mungu alimsimamisha Ibrahimu kwa wakati mwafaka. Kwake Mungu, utiifu wa Ibrahimu ulikuwa tayari umepita mtihani, kile alichofanya kilitosha, naye Mungu tayari alikuwa ameona matokeo ya kile Alichokuwa amenuia kufanya. Je, matokeo haya yalimtosheleza Mungu? Yaweza kusemekana kwamba matokeo haya yalimtosheleza Mungu na kwamba ndiyo ambayo Mungu alitaka, na ndiyo ambayo Mungu alikuwa ametamani kuyaona. Je, hili ni kweli? Ingawaje, katika miktadha tofauti, Mungu anatumia njia tofauti za kupima kila mtu. Kwa Ibrahimu Mungu aliona kile Alichotaka, Aliona kwamba moyo wa Ibrahimu ulikuwa wa kweli, na kwamba utiifu wake haukuwa na masharti na ilikuwa hali hii hasa ya “kutokuwa na masharti” ambayo Mungu alitamani. Watu mara nyingi husema, tayari nimetoa hii, tayari nimeachana na ile—kwa nini bado Mungu hajatosheka na mimi? Kwa nini Anaendelea kuniweka katika majaribio? Kwa nini Anaendelea kunijaribu? Hii yaonyesha ukweli mmoja: Mungu bado hajauona moyo wako, na bado hajapata moyo wako. Hivi ni kusema, Hajauona uaminifu kama wakati ule ambao Ibrahimu aliweza kukiinua kisu chake ili kumuua mtoto wake kwa mkono wake mwenyewe na kumtoa kwa Mungu. Bado Hajauona utiifu wako usio na masharti, na hajatulizwa na wewe. Ni jambo la kiasili, hivyo basi, kwamba Mungu anaendelea kukujaribu. Je, haya si kweli? Tutaachia hapa kwa mada hii. Halafu, tutasoma “Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu.”

3. Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu

Mwa 22:16-18 Mimi nimeapa kujipitia, akasema Yehova, kwa maana umefanya jambo hili, na hujamzuilia mwana wako, mwana wako wa pekee: Kuwa katika kubariki nitakupa baraka, na katika kuzidisha uzao wako nitazidisha mithili ya nyota za mbinguni, na mithili ya mchanga uliopo kwenye ukanda wa pwani; na uzao wako utakuwa na mlango wa maadui zao; Na kupitia uzao wako kila taifa la dunia litabarikiwa; kwa kuwa umeitumikia sauti Yangu.

Huu ni ukamilifu wa maelezo ya baraka za Mungu kwa Ibrahimu. Ingawaje ni fupi, maudhui yake ni mengi: Yanajumuisha sababu ya, na usuli wa, zawadi ya Mungu kwa Ibrahimu, na kile ambacho Alimpa Ibrahimu. Unao pia mhemko wa furaha na msisimko Aliotumia Mungu kutamka maneno haya, pamoja na haraka ya tamanio Lake la kupata wale wanaoweza kusikiliza maneno Yake. Katika haya, tunaona upendo wa Mungu kwa, na wema Wake kwa, wale wanaotii maneno Yake na kufuata amri Zake. Hivyo, pia, tunaiona gharama Anayolipia ili kupata watu, na utunzaji na fikira Anazotumia kuweza kuwapata. Zaidi ya hayo, kifungu hicho, kilicho na maneno “Mimi nimeapa kujipitia,” kinatupa hali ya nguvu ya machungu na maumivu Aliyoyapitia Mungu, na Mungu pekee, usiri wa kazi hii ya mpango wa usimamizi. Ni kifungu cha kuchokonoa fikira, na kile ambacho kilikuwa na umuhimu maalum kwa, na ilikuwa na athari nyingi ajabu kwa wale waliokuja baadaye.

Binadamu Anapata Baraka za Mungu kwa Sababu ya Uaminifu na Utii Wake

Je, baraka aliyopewa Ibrahimu na Mungu tuliyoisoma hapa ni kubwa? Ilikuwa kubwa vipi? Kunayo sentensi moja muhimu hapa: “Na kupitia uzao wako kila taifa la dunia litabarikiwa,” ambayo inaonyesha kwamba Ibrahimu alizipokea baraka ambazo hazikupewa tena kwa mwingine aliyekuja kabla au baadaye. Wakati, alipoulizwa na Mungu, Ibrahimu alimrudisha mwana wake wa pekee—mtoto wake pekee wa kiume na mpendwa Isaka—kwa Mungu (dokezo: Hapa hatuwezi kutumia neno “tolewa sadaka”; tunafaa kusema alimrudisha mtoto wake kwa Mungu), Mungu naye hakumruhusu tu Ibrahimu kutoa Isaka, lakini pia Alimbariki. Ni kwa ahadi gani Alimbariki Ibrahimu? Ahadi ya kuzidisha watoto wake. Na walizidishwa mara ngapi? Maandiko yanatuelezea rekodi hii: “... mithili ya nyota za mbinguni, na mithili ya mchanga uliopo kwenye ukanda wa pwani; na uzao wako utakuwa na mlango wa maadui zao; Na kupitia uzao wako kila taifa la dunia litabarikiwa.” Mungu Aliyatamka maneno haya katika muktadha upi? Hivi ni kusema, ni vipi ambavyo Ibrahimu alipokea baraka za Mungu? Alizipokea kama vile tu Mungu anavyosema kwenye maandiko: “kwa kuwa umeitumikia sauti Yangu.” Yaani, kwa sababu Ibrahimu alikuwa amefuata amri ya Mungu, kwa sababu alikuwa amefanya kila kitu ambacho Mungu alikuwa amesema, kuomba na kuamuru bila ya malalamiko hata kidogo, hivyo Mungu akatoa ahadi hiyo kwake. Kunayo sentensi moja muhimu katika ahadi hii ambayo inagusia fikira za Mungu wakati huo. Je, mmeiona? Huenda hamkutilia maanani sana maneno ya

Mungu kwamba “Mimi nimeapa kujipitia.” Yale yanamaanisha ni kwamba, wakati Mungu alipoyatamka maneno haya, Alikuwa anajiapisha Mwenyewe. Watu huapa kwa yapi wakati wanapokula kiapo? Wanaapa kwa Mbingu, hivi ni kusema, wanakula kiapo na jina la Mungu na kuapa kwa jina la Mungu. Huenda watu wasiwe na uelewa mwingi wa hali hiyo ambayo Mungu Alijiapisha mwenyewe, lakini mtaweza kuelewa Nitakapowapatia maelezo sahihi. Kukabiliwa na mtu ambaye aliweza tu kuyasikia maneno Yake lakini kutoelewa moyo Wake kwa mara nyingine kulimfanya Mungu kuhisi mpweke na mwenye upungufu. Katika hali ya kukata tamaa—na, yaweza kusemekana, kwa nadhari—Mungu alifanya kitu cha kiasili sana: Mungu aliuweka mkono Wake kwenye moyo wake na kutamka ahadi ya zawadi kwa Ibrahimu kwake Yeye Mwenyewe, na kutokana na haya binadamu akamsikia Mungu akisema “Mimi nimeapa kujipitia.” Kupitia vitendo vya Mungu, unaweza kujifikiria wewe mwenyewe. Unapoweka mkono wako juu ya moyo wako, na kujizungumzia, unalo wazo wazi kuhusu kile unachosema? Je, mwelekeo wako ni wa uaminifu? Unaongea waziwazi, kwa kutumia moyo wako? Hivyo, tunaona hapa kwamba wakati Mungu alipomzungumzia Ibrahimu, Alikuwa mwenye bidii na wa ukweli. Wakati huohuo alipokuwa Akiongea naye Ibrahimu na Akimbariki, Mungu alikuwa pia Akijizungumzia Mwenyewe. Alikuwa Akijiambia: Nitambariki Ibrahimu na kuuzidisha uzao wake kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani, kwa sababu alitii maneno Yangu na ndiye Niliyemchagua. Wakati Mungu aliposema “Mimi nimeapa kujipitia,” Mungu Aliamua kwamba ndani ya Ibrahimu Angezalisha wateule wa Israeli, na baadaye Angewaongoza watu hawa kusonga mbele sambamba na kazi Yake. Yaani, Mungu angekifanya kizazi cha Ibrahimu kufanya kazi ya usimamizi wa Mungu, na kazi ya Mungu na ile iliyoonyeshwa na Mungu ingeanza na Ibrahimu, na kuendelea katika vizazi vya Ibrahimu, na hivyo kuthamini tamanio la Mungu la kuokoa binadamu. Mnasemaje, hiki si kitu kilichobarikiwa? Kwa binadamu, hakuna baraka kubwa zaidi kuliko hii; hii, inaweza kusemekana, ndiyo baraka kubwa zaidi. Baraka aliyopata Ibrahimu haikuwa kuzidishwa kwa uzao wake, lakini ilikuwa Mungu kutimiza usimamizi Wake, agizo Lake na kazi Yake kwa vizazi vya Ibrahimu. Hii inamaanisha kwamba baraka alizopata Ibrahimu hazikuwa za muda, lakini ziliendelea kwa kadri mpango wa usimamizi wa Mungu ulipoendelea. Wakati Mungu alipoongea, wakati Mungu alipoapa kwa nafsi Yake Mwenyewe, tayari Alikuwa ameamua. Je, mchakato wa uamuzi huu ulikuwa kweli? Ulikuwa halisi? Mungu aliamua kwamba, kuanzia hapo kuendelea, jitihada Zake, gharama Aliyolipia, kile Anacho na alichu, kila kitu Chake, na hata maisha Yake yangekabidhiwa Ibrahimu na vizazi vya Ibrahimu. Na ndivyo pia Mungu alivyoamua kwamba, kuanzia kwenye kundi hili la watu, Angeonyesha vitendo Vyake, na kumruhusu binadamu kuiona hekima, mamlaka na nguvu Yake.

Kuwapata Wale Wanaomjua Mungu na Wanaoweza Kumshuhudia Ndilo Tamanio la

Mungu Lisilobadilika

Wakati huohuo Alipokuwa akijizungumzia Mwenyewe, Mungu alizungumza pia na Ibrahimu, lakini mbali na kusikiliza baraka ambazo Mungu alimpa, Ibrahimu aliweza kuyaelewa matamania ya kweli ya Mungu katika maneno Yake yote wakati huo? Hakuweza! Na hivyo, kwa wakati huo, wakati Mungu alipoapa kwa nafsi Yake Mwenyewe, moyo Wake ulikuwa bado pweke na wenye huzuni. Hakukuwepo hata na mtu mmoja wa kuweza kuelewa au kufahamu kile Alichonuia na Alichopangilia. Wakati huo, hakuna—akiwemo Ibrahimu—aliyeweza kuongea na Yeye kwa ujasiri, isitoshe hakuna yule aliyeweza kushirikiana na Yeye katika kufanya kazi ambayo lazima Angefanya. Juujuu, Mungu alikuwa Amempata Ibrahimu na Alipata mtu ambaye angetii maneno Yake. Lakini kwa hakika, maarifa ya mtu huyu kuhusu Mungu yalikuwa kidogo mno. Hata ingawaje Mungu alikuwa amembariki Ibrahimu, moyo wa Mungu ulikuwa bado hujatosheka. Inamaanisha nini kwamba Mungu hakuwa ametosheka? Inamaanisha kwamba usimamizi Wake ulikuwa tu umeanza, inamaanisha kwamba watu Aliotaka kupata, watu Aliotamani kuona, watu Aliopenda, walikuwa bado mbali na Yeye; Alihitaji muda, Alihitaji kusubiri, Alihitaji kuwa na subira. Kwani kwa wakati huo, mbali na Mungu Mwenyewe, hakuna yeyote yule aliyejua kile Alichohitaji au kile Alichotaka kupata, au kile Alichotamani. Na hivyo basi, Kwa wakati huohuo aliokuwa akihisi sana furaha Mungu pia alihisi kuwa mwenye uzito wa moyo. Bado Hakusitisha hatua Zake, na Aliendelea kupanga hatua inayofuata ya kile ambacho lazima Afanye.

Mnaona nini katika ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu? Mungu alimpa baraka kuu Ibrahimu kwa sababu tu ya yeye kusikiliza maneno ya Mungu. Ingawaje, juujuu, hali hii yaonekana ya kawaida na suala ambalo bila shaka, ndani yake tunauona moyo wa Mungu: Mungu hasa anathamini utiifu wa binadamu kwake Yeye, na hutunzwa mno na uelewa wa binadamu kuhusu Yeye na uaminifu wake Kwake. Mungu anathamini kiasi kipi uaminifu huu? Huenda msielewe ni kiasi kipi ambacho Yeye Anathamini, na huenda hata kusiwe na yeyote anayeutambua. Mungu alimpa Ibrahimu mwana, na wakati mwana huyo alipokua, Mungu alimwomba Ibrahimu kumkabidhi mtoto wake Kwake. Ibrahimu alifuata amri ya Mungu kwa umakinifu, alitii neno la Mungu na uaminifu wake ulimpendeza Mungu na ukathaminiwa sana na Mungu. Mungu aliuthamini kiasi kipi? Na kwa nini Akathamini sana? Kwa wakati ambao hakuna aliyefahamu maneno ya Mungu au kuelewa moyo Wake, Ibrahimu alifanya kitu kilichotikisa mbingu na kutetemesha ardhi, na kikafanya Mungu kuhisi hali fulani ya kutosheka kwa mara ya kwanza, kikamletea Mungu furaha ya kumpata mtu ambaye aliweza kutii maneno Yake. Ridhaa na furaha hii ilitoka kwa kiumbe aliyeumbwa kwa mikono ya Mungu, na ndiyo iliyokuwa “sadaka” ya kwanza ambayo binadamu aliwahi kumpa Mungu na ambayo ilithaminiwa sana na Mungu, tangu binadamu kuumbwa. Mungu alikuwa na wakati mgumu kusubiria sadaka hii, na Aliichukulia

kama zawadi ya kwanza muhimu zaidi kutoka kwa binadamu, ambaye Alikuwa amemuumba. Hii ilionyesha Mungu tunda la kwanza la jitihada Zake, na gharama ambayo Alikuwa amelipia na ikamruhusu Yeye kuliona tumaini kwa wanadamu. Baadaye, Mungu alikuwa na hata tamanio kubwa zaidi la kundi la watu kama hao wa kushinda na Yeye kumchukulia Yeye kwa uaminifu, kumtunza Yeye kwa uaminifu. Mungu alitamani hata kwamba Ibrahimu angeendelea kuishi, kwani Alipenda kuwa na moyo kama huo ukiandamana na Yeye na kuwa na Yeye Alipoendelea na usimamizi Wake. Haijalishi ni nini alichotaka Mungu, yalikuwa tu ni matakwa, wazo tu—kwani Ibrahimu alikuwa tu binadamu aliyeweza kumtii Yeye, na wala hakuwa na uelewa au maarifa hata madogo zaidi kuhusu Mungu. Yeye alikuwa mtu aliyepungukiwa pakubwa na viwango vya mahitaji ya Mungu kwa binadamu: kumjua Mungu, kuweza kushuhudia Mungu, na kuwa na akili sawa na Mungu. Na hivyo, hangeweza kutembea na Mungu. Katika sadaka ya Ibrahimu ya Isaka, Mungu aliuona uaminifu na utiifu huu wa Ibrahimu, na Akaona kwamba alikuwa amestahimili jaribio la Mungu kwake yeye. Hata ingawaje Mungu aliukubali uaminifu na utiifu wake, bado hakustahili kuwa mwandani wa Mungu, wa kuwa mtu aliyemjua Mungu, na kumwelewa Mungu, na alifahamishwa kuhusu tabia ya Mungu; alikuwa mbali sana na kuwa na akili sawa na Mungu na vilevile kuweza kufanya mapenzi ya Mungu. Hivyo basi, katika moyo Wake, Mungu alikuwa bado mpweke na mwenye wasiwasi. Kwa kadri Mungu alipokuwa mpweke na mwenye wasiwasi zaidi, ndipo Yeye alipohitaji zaidi kuendelea na usimamizi Wake haraka iwezekanavyo, na kuweza kuchagua na kulipata kundi la watu wa kukamilisha mpango Wake wa usimamizi na kutimiza mapenzi Yake haraka iwezekanavyo. Hili ndilo lilikuwa tamanio lenye hamu kubwa la Mungu, na limebakia vilevile kuanzia mwanzo kabisa hadi leo. Tangu Alipomuumba binadamu hapo mwanzo, Mungu ametamani kuwa na kundi la washindi, kundi ambalo litatembea na Yeye na linaweza kuelewa, kujua na kufahamu tabia Yake. Mapenzi haya ya Mungu hayajawahi kubadilika. Haijalishi ni muda gani bado Atasubiria, haijalishi barabara iliyo mbele ni ngumu kiasi gani, hata malengo Anayoyatamani yawe mbali kiasi kipi, Mungu hajawahi kubadilisha au kukata tamaa katika matarajio Yake kuhusu binadamu. Kwa vile nimeyasema haya, mnatambua chochote kuhusu mapenzi ya Mungu? Pengine kile ulichotambua hakina uzito sana—lakini kitajitokeza kwa utaratibu!

Katika kipindi sawa na kile cha Ibrahimu, Mungu pia aliliangamiza jiji. Jiji hili liliitwa Sodom. Bila shaka, watu wengi wanaijua hadithi ya Sodom, lakini hakuna yeyote aliyejua fikira za Mungu zilikuwa usuli wa kuangamiza Kwake jiji hili.

Na hivyo leo, kupitia mazungumzo yake Mungu na Ibrahimu hapa chini, tutajifunza fikira Zake wakati huo, huku pia tukijifunza kuhusu tabia Yake. Kinachofuata, hebu tusome vifungu vya maandiko.

B. Mungu Lazima Aangamize Sodoma

Mwa 18:26 Na Yehova akasema, Nikipata katika Sodoma watu hamsini wenye haki ndani ya mji huo, basi nitaacha pahali pote kwa sababu yao.

Mwa 18:29 Na akanena tena na Yeye, na kusema, Iwapo watu arobaini wakapatikana humo. Naye Akasema, Sitafanya hivyo kwa sababu yao.

Mwa 18:30 Na akamwambia, Iwapo watapatikana huko watu thelathini. Naye Akasema, Sitafanya hivyo kwa sababu yao.

Mwa 18:31 Na akasema, Iwapo watapatikana huko watu ishirini. Naye Akasema, Sitauharibu kwa sababu yao.

Mwa 18:32 Na akasema, Iwapo watapatikana huko watu kumi. Naye Akasema, Sitauharibu kwa sababu yao.

Hizi ni dondoo chache Nilizochagua kutoka kwenye Biblia. Dondoo hizi si kamilifu, za matoleo ya awali. Kama mngependa kuziona hizo, mnaweza kuzitafuta kwenye Biblia nyinyi wenyewe; ili kuokoa muda, Nimeiacha sehemu ya maudhui asilia. Hapa Nimechagua tu vifungu na sentensi mbalimbali kuu, huku nikiziacha sentensi mbalimbali ambazo hazina umuhimu katika ushirika wetu wa leo. Katika vifungu na maudhui yote tunayotumia katika ushirika, zingatia letu haliyaendei maelezo ya hadithi na mwenendo wa binadamu katika hadithi hizi; badala yake, tunazungumzia tu fikira za Mungu na mawazo Yake wakati huo. Katika fikira na mawazo ya Mungu, tutaiona tabia ya Mungu, na kutoka katika kila kitu alichofanya Mungu, tutaweza kumuona Mungu Mwenyewe wa kweli—na katika haya tutaweza kutimiza malengo yetu.

Mungu Anawajali tu Wale Wanaoweza Kutii Maneno Yake Na Kufuata Amri Zake

Vifungu hivi vilivyotajwa hapo juu vinayo maneno msingi mbalimbali: nambari. Kwanza, Yehova alisema kwamba kama Angewapata wenye haki hamsini ndani ya Jiji, basi Angepanusurisha mahali hapo, hii ni kusema, Asingeangamiza jiji hilo. Hivyo walikuwepo, kwa hakika, watakatifu hamsini ndani ya Sodoma? Hawakuwemo. Muda mfupi baadaye, Ibrahimu alimwambia nini Mungu? Alisema, labda kutakuwemo arubaini waliopatikana humo? Naye Mungu akasema, Sitafanya hivyo. Kisha, Ibrahimu akasema huenda wakawepo thelathini watakaopatikana hapo? Naye Mungu akasema, Sitafanya hivyo. Na labda ishirini? Sitafanya hivyo. Kumi? Sitafanya hivyo. Kulikuwemo, kwa hakika, wenye haki kumi ndani ya jiji? Hapakuwa kumi—lakini kulikuwemo na mmoja. Na huyu mmoja alikuwa nani? Alikuwa Loti. Wakati huo, kulikuwepo tu na mwenye haki mmoja kwenye eneo la Sodoma, lakini Mungu

alikuwa amemakinika sana au mkali kuhusiana na nambari hii? La, hakuwa hivyo! Na wakati binadamu aliendelea kuulizia, “Na je wale arubaini?” “Na je wale thelathini?” mpaka pale alipofika katika sehemu ile ya “Na je wale kumi?” Mungu alisema, “Hata kama wanalikuwemo kumi, Singeangamiza jiji hilo; Ningelinusurisha, na kuwasamehe wale watu wengine mbali na wale kumi.” Idadi ya watu kumi ingekuwa ya kuhurumiwa vya kutosha, lakini ilitokea kwamba, kwa hakika, hakukuwemo na hata ile idadi inayohitajika ya watu wenye haki kule Sodoma. Unaona, basi, kwamba katika macho ya Mungu dhambi na maovu ya watu wa jiji ilikuwa kwa kiasi kwamba Mungu hakuwa na chaguo lolote ila kuwaangamiza. Mungu alimaanisha nini Aliposema kwamba Asingeliharibu jiji kama kungekuwemo na wenye haki hamsini? Nambari hizi hazikuwa muhimu kwa Mungu. Kile kilichokuwa muhimu kilikuwa kama jiji lilikuwa na wenye haki Aliotaka au la. Kama jiji lisingekuwa na mwenye haki yeyote isipokuwa mmoja, Mungu asingeruhusu madhara kuwepo kutokana na Yeye kuangamiza jiji hilo. Kile ambacho haya yote yanamaanisha ni kwamba, haijalishi kama Mungu angeliangamiza jiji au la, na haijalishi idadi ya wenye haki waliokuwa ndani ya jiji hilo, kwake Mungu jiji hili lenye dhambi lilikuwa limelaaniwa na lilikuwa limejaa maovu, na hivyo lilifaa kuangamizwa, na kutoweka kwenye macho ya Mungu huku nao wenye haki wakisali. Haikulijalisha enzi husika, haikujalisha awamu ya maendeleo ya wanadamu, mwelekeo wa Mungu haubadiliki: Anachukia maovu, na Anawajali wenye haki mbele ya macho Yake. Mwelekeo huu wazi wa Mungu ndiyo pia ufunuo wa kweli wa kiini cha Mungu. Kwa sababu hakukuwepo na mwenye haki yeyote isipokuwa mmoja ndani ya jiji, Mungu hakusita tena. Matokeo yake ni kwamba Sodoma ingeangamizwa bila kusita. Mnaona nini katika haya? Katika enzi hiyo, Mungu asingeangamiza jiji kama wamo wenye haki hamsini ndani yake, wala kama kulikuwemo kumi, kumaanisha kwamba Mungu angeamua kusamehe na kumvumilia wanadamu, au angefanya kazi ya kuongoza, kwa sababu ya watu wachache ambao waliweza kumstahi na kumwabudu Yeye. Mungu hutilia maanani haki ya binadamu, Hutilia maanani sana kwa wale wanaoweza kumwabudu Yeye, na Anatilia maanani sana wale wanaoweza kufanya matendo mema mbele yake.

Kutoka nyakati za mapema sana hadi leo, umewahi kusoma ndani ya Biblia kuhusu Mungu kuuwasilisha ukweli, au kuzungumzia kuhusu njia ya Mungu, kwa mtu yeyote? La, hujawahi. Maneno ya Mungu kwa binadamu tunayoyasoma yaliwaambia watu tu cha kufanya. Baadhi walienda na wakayafanya, baadhi hawakuyafanya; baadhi walisadiki, na baadhi hawakusadiki. Hivyo ndivyo ilivyokuwa tu. Hivyo, wenye haki wa enzi hiyo—wale waliokuwa wenye haki mbele ya macho ya Mungu—walikuwa wale tu ambao wangeweza kuyasikia maneno ya Mungu na kufuata amri za Mungu. Walikuwa watumishi waliotekeleza maneno ya Mungu miongoni mwa binadamu. Je, watu kama hao wangeweza kuitwa wale wanaomjua Mungu? Wangeweza kuitwa watu waliofanywa kuwa watimilifu na Mungu? La, wasingeweza kuitwa hivyo. Na

hivyo, licha ya idadi yao, kwenye macho ya Mungu hawa watu wenye haki walistahili kuitwa wandani wa Mungu? Wangeweza kuitwa mashahidi wa Mungu? Bila shaka la! Hawakustahili kamwe kuitwa wandani na mashahidi wa Mungu. Na hivyo Mungu aliwaita watu kama hawa vipi? Kwenye Biblia, hadi kufikia kwenye vifungu vya maandiko ambavyo tumetoka kusoma hivi punde, kulikuwa na matukio mengi ya Mungu kuwaita “Mtumishi wangu.” Hivi ni kusema, kwa wakati huo kwenye macho ya Mungu watu hawa wenye haki walikuwa watumishi wa Mungu, walikuwa watu waliomhudumia Yeye duniani. Naye Mungu alifikiria vipi kuhusu jina hilo? Kwa nini Akawaita hivyo? Je, Mungu anavyo viwango ambavyo Anatumia katika Kuwaita watu ndani ya moyo Wake? Bila shaka anavyo. Mungu anavyo viwango, haijalishi kama Anawaita watu wenye haki, watimilifu, wanyofu, au watumishi. Anapomwita mtu mtumishi Wake, Anayo imani thabiti kwamba mtu huyu anaweza kuwapokea wajumbe Wake, na anaweza kufuata amri Zake, na anaweza kutekeleza kile ambacho ameamrisha kufanya na wale wajumbe. Na mtu huyu anatekeleza nini? Kile ambacho Mungu anamwamuru binadamu kufanya na kutekeleza duniani. Wakati huo, kile ambacho Mungu alimwomba binadamu kufanya na kutekeleza duniani kingeweza kuitwa njia ya Mungu? La, kisingeweza. Kwani wakati huo, Mungu alimwomba tu binadamu kufanya mambo machache rahisi; Alitamka amri chache rahisi, Akimwambia binadamu kufanya hiki au kile, na si zaidi ya hayo. Mungu alikuwa akifanya kazi kulingana na mpango Wake. Kwa sababu, wakati huo, masharti mengi hayakuwepo, muda ulikuwa haujatimia, na ilikuwa vigumu kwake wanadamu kuvumilia njia ya Mungu, hivyo basi njia ya Mungu ilikuwa bado haijaanza kuwasilishwa mbele kutoka kwenye moyo wa Mungu. Katika haya, tunaona kwamba haijalishi kama kulikuwa thelathini au ishirini ya wale wenye haki aliozungumzia Mungu, mbele ya macho Yake wote walikuwa watumishi Wake. Wakati wajumbe wa Mungu walipowajia watumishi hawa, wangeweza kuwapokea, na kufuata amri zao, na kutenda kulingana na maneno yao. Haya ndiyo hasa yaliyofaa kufanywa, na kutimizwa, na wale waliokuwa watumishi mbele ya macho ya Mungu. Mungu ni mwenye busara katika majina Yake kwa watu. Si kwa sababu walikuwa vile mlivyo sasa ndiyo Aliwaita watumishi Wake—si kwa sababu walikuwa wamesikia mahubiri mengi, walijua kile ambacho Mungu alifaa kufanya, walielewa mengi kuhusu mapenzi ya Mungu na walifahamu mpango Wake wa usimamizi—lakini kwa sababu walikuwa waaminifu katika ubinadamu wao na waliweza kutii maneno ya Mungu; wakati Mungu alipowaamuru, waliweza kuweka pembeni kile walichokuwa wakifanya na kutekeleza kile ambacho Mungu aliwaamuru kufanya. Hivyo, kwake Mungu safu ile nyingine ya maana kwenye cheo cha mtumishi ni kwamba walishirikiana na kazi Yake duniani na ingawaje hawakuwa wajumbe wa Mungu, hao ndio waliokuwa watekelezaji na wafuatiliaji wa maneno ya Mungu duniani. Unaona, basi, watumishi hawa au wenye haki hawa walikuwa na umuhimu mkubwa katika moyo wa Mungu. Kazi ile ambayo Mungu alifaa kuishughulikia duniani isingeweza kufanyika bila ya watu wa kushirikiana na Yeye, na wajibu uliotekelwa na

watumishi wa Mungu usingeweza kufanywa na wajumbe wa Mungu. Kila kazi ambayo Mungu alitoa amri kwa watumishi hawa ilikuwa yenye umuhimu mkubwa Kwake, na hivyo basi Asingeweza kuwapoteza. Bila ya ushirikiano wa watumishi hawa na Mungu, kazi Yake miongoni mwa wanadamu ingefikia kikomo, na matokeo yake ni kwamba mpango wa usimamizi wa Mungu na matumaini ya Mungu vyote visingewezekana.

Mungu ni Mwenye Wingi wa Rehema Kwa Wale Anaowajali, na Mwenye Hasira Kali kwa Wale Anaowachukia na Kukataa

Katika simulizi za Biblia, kulikuwepo na watumishi kumi wa Mungu kule Sodoma? La, hakukuwepo! Kulikuwepo na jiji lililostahili kusamehewa na Mungu? Mtu mmoja tu kwenye jiji hilo—Loti—ndiye aliye wapokea wajumbe wa Mungu. Matokeo ya haya ni kwamba kulikuwa na mtumishi mmoja tu wa Mungu kwenye jiji, na hivyo basi Mungu hakuwa na chaguo ila kumwokoia Loti na kuliangamiza jiji la Sodoma. Mabadilishano haya kati ya Ibrahimu na Mungu yanaweza kuonekana kuwa rahisi tu, lakini yanaonyesha kitu fulani kikuu: Kuna kanuni za vitendo vya Mungu, na kabla ya kufanya uamuzi Atachukua muda mrefu akiangalia na kutafakari; kabla ya wakati kuwa sawa, bila shaka Hatafanya au kukimbilia hitimisho zozote. Mabadilishano kati ya Ibrahimu na Mungu yanatuonyesha kwamba uamuzi wa Mungu wa kuangamiza Sodoma haukuwa mbaya hata kidogo, kwani Mungu alijua tayari kwamba kwenye jiji hakukuwa na watu arubaini wenye haki, na wala thelathini wenye haki, wala ishirini. Hawakuwa hata kumi. Mtu mwenye haki pekee kwenye jiji alikuwa Loti. Yote yaliyofanyika ndani ya Sodoma na hali zake ziliangaliwa na Mungu, na zilizoeleka kwa Mungu kama sehemu ya nyuma ya mkono Wake. Hivyo, uamuzi Wake usingekosa kuwa sahihi. Kinyume na haya, tukilinganisha uweza wa Mungu, binadamu hajali katu, ni mjinga na asiyejua neno, asiyeona mbali katu. Haya ndiyo tunayoona katika mabadilishano kati ya Ibrahimu na Mungu. Mungu amekuwa akiwasilisha mbele tabia Yake kuanzia mwanzo hadi leo. Hapa, vilevile, kuna pia tabia ya Mungu tunayofaa kuona. Nambari ni rahisi, na hazionyeshi chochote, lakini hapa kuna maonyesho muhimu sana ya tabia ya Mungu. Mungu asingeangamiza jiji kwa sababu ya watu hamsini wenye haki. Je, haya ni kutokana na rehema ya Mungu? Ni kwa sababu ya upendo na uvumilivu Wake? Je mmeuona upande huu wa tabia ya Mungu? Hata kama kungekuwa na wenye haki kumi pekee, Mungu asingeangamiza jiji hili kwa sababu ya watu hawa kumi wenye haki. Je, haya yanaonyesha uvumilivu na upendo wa Mungu au la? Kwa sababu ya rehema, uvumilivu, na kujali kwa Mungu kwa wale watu wenye haki, Asingeliangamiza jiji hili. Huu ndio uvumilivu wa Mungu. Na hatimaye, ni matokeo gani tunayoyaona? Wakati Ibrahimu aliposema, “Iwapo watapatikana huko watu kumi,” Mungu akasema, “Sitauharibu kwa sababu yao.” Baada ya hapo, Ibrahimu hakusema tena—kwani ndani ya Sodoma hakukuwa na wenye haki kumi aliwarejelea, na hakuwa na chochote ziada cha kusema, na kwa wakati huo alielewa

ni kwa nini Mungu alikuwa ameamua kuangamiza Sodoma. Katika haya, ni tabia gani ya Mungu unayoiona? Ni aina gani ya utatuzi ambayo Mungu alifanya? Yaani, kama jiji hili lisingekuwa na wenye haki kumi, Mungu asingeruhusu uwepo wake, na bila shaka Angeliangamiza. Je hii si hasira ya Mungu? Je, hasira hii inawakilisha tabia ya Mungu? Je, hii tabia ni ufunuo wa kiini cha haki cha Mungu? Je, huu ni ufunuo wa kiini cha haki ya Mungu, ambacho binadamu hafai kukosea? Baada ya kuthibitisha kwamba hakukuwa na wenye haki kumi kule Sodoma, Mungu alikuwa na hakika ya kuliangamiza jiji, na angewaadhibu vikali watu walio ndani ya hilo jiji, kwani walimpinga Mungu, na kwa sababu walikuwa wachafu na waliopotoka.

Kwa nini tumechambua vifungu hivi kwa njia hii? Kwa sababu sentensi hizi chache rahisi zinatupa maonyesho kamili ya tabia ya Mungu ya wingi wa rehema na hasira kali. Wakati sawa na kuthamini sana wale wenye haki na kuwa na rehema juu yao, kuwavumilia, na kuwajali, ndani ya moyo wa Mungu kulikuwa na chukizo kuu kwa wale waliokuwa ndani ya Sodoma ambao walikuwa wamepotoshwa. Je, hii ilikuwa, au haikuwa rehema nyingi na hasira kali? Ni kwa mbinu zipi Mungu aliliangamiza jiji? Kwa moto. Na kwa nini Aliliangamiza kwa kutumia moto? Unapooni kitu kikiungua kwa moto, au wakati uko karibu kuchoma kitu, ni nini hisia zako juu ya kitu hicho? Kwa nini unataka kukichoma? Unahisi kwamba hukihitaji tena, kwamba hutaki tena kukiangalia? Unataka kukiacha? Matumizi ya moto na Mungu yanamaanisha uwachaji, na chuki, na kwamba hakutaka tena kuiona Sodoma. Hii ilikuwa ni hisia iliyomfanya Mungu kuteketeza Sodoma kwa moto. Matumizi ya moto yanawakilisha namna ambavyo Mungu alikuwa amekasirika. Rehema na uvumilivu wa Mungu kwa kweli vipo, lakini utakatifu na uhaki wa Mungu Anapoachilia hasira Yake pia inaonyesha binadamu upande wa Mungu usiyovumilia kosa lolote. Wakati binadamu anaweza kabisa kutii amri za Mungu na kutenda kulingana na mahitaji ya Mungu, Mungu anakuwa mwingi katika huruma Yake kwa binadamu; wakati binadamu amejawa na upotoshaji, chuki na uadui kwake Yeye, Mungu anakuwa mwenye ghadhabu nyingi. Na anakuwa na ghadhabu nyingi hadi kiwango kipi? Hasira yake itaendelea kuwepo mpaka pale ambapo Mungu hataona tena upinzani wa binadamu na matendo maovu, mpaka vyote hivi havipo tena mbele ya macho Yake. Hapo tu ndipo ghadhabu ya Mungu itakapotoweka. Kwa maneno mengine, haijalishi mtu husika ni yupi, kama moyo wake umekuwa mbali na Mungu, na yeye amemgeukia Mungu, asirudi tena, basi haijalishi ni vipi, kwa mwonekano wote au kuhusiana na matamano yake ya kibinafsi, atapenda kuabudu na kufuata na kutii Mungu katika mwili wake au katika kufikiria kwake pindi tu moyo wake utakapokuwa mbali na ule wa Mungu, hasira ya Mungu itaachiliwa bila kikomo. Itakuwa kwamba wakati Mungu anapoiachilia kabisa ghadhabu Yake, akiwa amempa binadamu fursa za kutosha, pindi inapoachiliwa hakutakuwepo na njia yoyote ya kuirudisha, na hatawahi tena kuwa mwenye huruma na mvumilivu kwa mtu kama huyo. Huu ni upande mmoja wa tabia ya Mungu

isiyovumilia kosa. Hapa, yaonekana kawaida kwa watu kwamba Mungu angeliangamiza jiji, kwani ndani ya macho ya Mungu, jiji lililojaa dhambi lisingeweza kuwepo na kuendelea kubakia pale, na lilikuwa jambo la kueleweka kwamba jiji hilo liangamizwe na Mungu. Lakini katika kile kilichofanyika kabla ya na kufuatia uangamizaji Wake wa Sodoma, tunaiona tabia nzima ya Mungu. Yeye ni mvumilivu na mwenye huruma kwa viumbe walio wenye wema na wazuri na wa kupendeza; kwa vitu viovu, na vyenye dhambi, na vilivyojaa maovu, Yeye anayo hasira kali, kiasi cha kwamba Hawachi kuendeleza hasira Yake. Hivi ndivyo vipengele viwili vikuu na vinavyojitokeza zaidi kuhusu tabia ya Mungu, na, zaidi, vimefichuliwa na Mungu kutoka mwanzo hadi mwisho: wingi wa huruma na ghadhabu nyingi. Wengi wenu mmepitia huruma ya Mungu, lakini wachache sana wameweza kutambua hasira ya Mungu. Huruma na upole wa upendo wa Mungu unaweza kuonekana kwa kila mmoja; yaani, Mungu Amekuwa mwingi wa huruma kwa kila mmoja. Ilhali ni nadra sana—au, inaweza kusemekana, kamwe—Mungu amekuwa na ghadhabu nyingi kwa watu binafsi au sehemu yoyote ya watu miongoni mwenu. Tulia! Hivi karibuni au baadaye, hasira ya Mungu itaonekana na kupitiwa na kila mmoja, lakini kwa sasa bado muda haujawadia. Na kwa nini hivi? Kwa sababu wakati Mungu anakuwa na ghadhabu kila mara kwa mtu, yaani, wakati Anapoiachilia hasira Yake kuu kwao, inamaanisha kwamba Amekuwa akichukia na Akikataa kwa muda mrefu mtu huyu, kwamba Anadharau uwepo wake na kwamba Hawezi kuvumilia uwepo wake; pindi tu ghadhabu Yake inapomjia, watatoweka. Leo, kazi ya Mungu bado haijafikia hapo. Hakuna yeyote kati yenu ambaye ataweza kuivumilia pindi tu Mungu anapoghadhabika kupindukia. Mnaona, kisha, kwamba kwa wakati huu Mungu anayo huruma nyingi tu kwa watu wote, na ungali hujaona ghadhabu yake nyingi. Kama wapo wale wanaobakia wakiwa hawajashawishika, mnaweza kuuliza kuwa hasira ya Mungu ije kwenu, ili mweze kuipitia na kujua kama ghadhabu ya Mungu na tabia Yake isiyokosewa kwa binadamu ipo kwa kweli au la. Mtathubutu kufanya hivyo?

Watu Wa Siku Za Mwisho Wanaiona tu Hasira Ya Mungu Katika Maneno Yake, na Hawaipitii kwa Kweli Hasira Ya Mungu

Je, pande mbili za tabia ya Mungu zinazoonekana kwenye vifungu hivi vya maandiko zinastahili ushirika? Baada ya kuisikia hadithi hii, je, mnao uelewa mpya kuhusu Mungu? Ni uelewa aina gani? Inaweza kusemekana kwamba kuanzia wakati wa uumbaji mpaka leo, hakuna kikundi ambacho kimefurahia neema au huruma nyingi za Mungu pamoja na upole wa upendo kama kikundi hiki cha mwisho. Ingawaje, kwenye awamu ya mwisho, Mungu amefanya kazi Yake ya hukumu na kuadibu, na Amefanya kazi Yake kwa adhama na hasira, wakati mwingi Mungu anatomia tu maneno kukamilisha kazi Yake; Anatomia maneno ili kufunza, kunyunyiza na kutosheleza, na kulisha. Hasira ya Mungu, wakati haya yakiendelea, siku zote imefichwa, na mbali na kuipitia tabia ya Mungu yenye hasira kwa maneno Yake, watu wachache sana

wamepitia ghadhabu Yake ana kwa ana. Hivi ni kusema, kwamba wakati wa kazi ya hukumu na kuadibu kwa Mungu, ingawaje hasira iliyofichuliwa katika maneno ya Mungu inawaruhusu watu kupitia adhama na kutovumilia kosa kwa Mungu, hasira hii haizidi maneno Yake. Kwa maneno mengine, Mungu hutumia maneno ili kukemea binadamu, kumfichua binadamu, kuhukumu binadamu, kumwadhibu binadamu na hata kumshutumu binadamu—lakini Mungu angali hajawa mwenye wingi wa ghadhabu kwa binadamu, na hata hajaachilia hasira Yake kwa binadamu nje ya maneno yake. Hivyo, rehema na upole wa upendo wa Mungu uliopitiwa na binadamu kwenye enzi hii ni ufunuo wa tabia ya kweli ya Mungu, huku hasira ya Mungu iliyoipitiwa na binadamu ikiwa tu ni athari ya sauti na hisia za matamko Yake. Watu wengi wanachukulia athari hii kimakosa na kuiona kuwa njia ya kweli ya kupitia na maarifa ya kweli ya hasira ya Mungu. Hivyo basi, watu wengi wanasadiki kwamba wameiona huruma ya Mungu na upole wa upendo ndani ya maneno Yake, kwamba wameweza pia kushuhudia kutovumilia Kwake kwa kosa la binadamu, na wengi wao wamekuja hata kutambua huruma na uvumilivu wa Mungu kwake binadamu. Haijalishi tabia ya binadamu ni mbaya kiasi kipi, au upotovu wa tabia yake, Mungu siku zote anavumiliwa. Katika kuvumiliwa, nia Yake ni kusubiria maneno Aliyokuwa Ametamka, jitihada Alizofanya na gharama Aliyolipia ili kutimiza athari iliyo ndani ya wale Anaotaka kupata. Kusubiria matokeo kama haya yanachukua muda, na yanahitaji uumbaji wa mazingira tofauti ya binadamu, kwa njia sawa ambayo watu hawawi watu wazima pindi tu wanapozaliwa; huchukua miaka kumi na minane au kumi na tisa na baadhi ya watu hata huhitaji miaka ishirini au thelathini kabla hawajakomaa na kuwa mtu mzima halisi. Mungu husubiria kukamilika kwa mchakato huu, Yeye husubiria kuwadia kwa muda huo, na Yeye husubiria kufika kwa matokeo haya. Na kwa muda wote Anaousubiria, Mungu huwa mwenye wingi wa huruma. Kwenye kipindi cha kazi ya Mungu, hata hivyo, kiwango kidogo sana cha watu kinaangamizwa, na baadhi wanaadhibiwa kwa sababu ya upinzani wao mkuu kwa Mungu. Mifano kama hiyo ni ithibati kubwa zaidi ya tabia ya Mungu ambayo haivumilii kosa la binadamu, na inathibitisha kabisa uwepo wa kweli wa uvumilivu na ustahimilivu wa Mungu kwa wale wateule. Bila shaka, katika mifano hii halisi, ufunuo wa sehemu ya tabia ya Mungu kwa watu hawa hauathiri jumla ya mpango wa usimamizi wa Mungu. Kwa hakika, kwenye awamu hii ya mwisho ya kazi ya Mungu, Mungu amevumilia kwenye kipindi hiki chote ambacho Amekuwa akisubiria na Amebadilisha uvumilivu Wake na maisha Yake kwa wokovu wa wale wanaomfuata Yeye. Mnayaona haya yote? Mungu haharibu mpango Wake bila sababu. Anaweza kuiachilia hasira Yake na Anaweza pia kuwa mwenye huruma; huu ndio ufunuo wa sehemu mbili kuu za tabia ya Mungu. Je, hii iko au haiko wazi kabisa? Kwa maneno mengine, tunapokuja kwa Mungu, sahihi na isiyokuwa sahihi, yenye haki na dhalimu, nzuri na mbaya—hivi vyote vimeonyeshwa waziwazi kwa binadamu. Kile Atakachofanya, kile Anachopenda, kile Anachochukia—yote haya yanaweza kuonyeshwa moja kwa moja katika tabia Yake. Mambo

kama hayo yanaweza pia kuwa ya waziwazi sana na ya kuonekana katika kazi ya Mungu na hayako juujuu au kwa jumla; badala yake, yanaruhusu watu wote kutazama tabia ya Mungu na kile Anacho na alichu hasa kwa njia thabiti, ya kweli na ya kimatendo. Huyu ndiye Mungu Mwenyewe wa kweli.

Tabia ya Mungu Haijawahi Kufichwa Kutoka Kwa Binadamu—Moyo wa Binadamu Umepotoka kwa Mungu

Kama Sikushiriki kuhusu mambo haya, hakuna yeyote kati yenu ambaye angeweza kutazama tabia ya kweli ya Mungu katika hadithi za Biblia. Hii ni ukweli. Hiyo ni kwa sababu, ingawaje hadithi hizi za kibiblia zilirekodi baadhi ya mambo ambayo Mungu alifanya, Mungu aliongea mambo machache na hakuitambulisha tabia Yake kwa njia ya moja kwa moja au kuwasilisha mbele waziwazi mapenzi Yake kwa binadamu. Vizazi vya baadaye vimechukulia rekodi hizi kama tu hadithi, na hivyo yaonekana kwa watu kwamba Mungu anajificha kutoka kwa binadamu na kwamba si nafsi ya Mungu ambayo imefichwa kutoka kwa binadamu, lakini tabia na mapenzi Yake. Baada ya ushirika wangu leo, bado mnahisi kwamba Mungu amefichwa kabisa kutoka kwa binadamu? Bado mnasadiki kwamba tabia ya Mungu imefichwa kutoka kwa binadamu?

Tangu wakati wa uumbaji, tabia ya Mungu imeenda sako kwa bako na kazi Yake. Haijawahi kufichwa kutoka kwa binadamu, lakini imewekwa kadamnasi na kwa dhahiri kabisa kwa binadamu. Ilhali, kwa kadri muda unavyopita, moyo wa binadamu umekua hata mbali zaidi na Mungu, na kwa kuwa upotovu wa mwanadamu umekuwa wa kina zaidi, binadamu na Mungu wamekuwa mbali na mbali zaidi kati yao. Kwa utaratibu lakini kwa uhakika, binadamu ametoweka kutoka kwa macho ya Mungu. Binadamu ameshindwa kuweza “kuona” Mungu, jambo ambalo limemwacha yeye bila “habari” zozote kuhusu Mungu; hivyo, hajui kama Mungu yupo, na hata anaenda mbali mno kiasi cha kukataa kabisa kuwepo kwa Mungu. Kwa hivyo, kutofahamu kwa binadamu kuhusu tabia ya Mungu, na kile Anacho na alichu, si kwa sababu Mungu amefichwa kutoka kwa binadamu, lakini kwa sababu moyo wake umemgeukia Mungu. Ingawaje binadamu anamsadiki Mungu, moyo wa binadamu haupo na Mungu, na hajui chochote kuhusu namna ya kumpenda Mungu, wala hataki kumpenda Mungu, kwani moyo wake haujawahi kusonga karibu na Mungu na siku zote anamuepuka Mungu. Kutokana na haya, moyo wa binadamu umekuwa mbali sana na Mungu. Kwa hivyo, moyo wake uko wapi? Kwa hakika, moyo wa binadamu haujaenda popote: Badala ya kuupatia moyo huo Mungu, au kuufichua kwa Mungu ili Aweze kuuona, amejiekea yeye mwenyewe. Hiyo ni licha ya ukweli kwamba baadhi mara nyingi wanamwomba Mungu na kusema, “Ee Bwana, utazame moyo wangu—unajua yote ninayofikiria,” na baadhi hata huapa kumruhusu Mungu kuwafikiria, kwamba waweze

kuadhibiwa kama watawunja kiapo chao. Ingawaje binadamu anamruhusu Mungu kuangalia ndani ya moyo wake, hii haimanishi kwamba anaweza kutii mipango na mipangilio ya Mungu, wala kwamba ameacha hatima na matarajio yake na mambo yake yote katika udhibiti wa Mungu. Hivyo, licha ya viapo unavyotoa kwa Mungu au mwelekeo kwake Yeye, kwa macho ya Mungu moyo wako ungali umefungwa kwake Yeye, kwani unamruhusu Mungu tu kuangalia kwenye moyo wako lakini humruhusu Yeye kuudhibiti. Kwa maneno mengine, hujampa Mungu moyo wako kamwe, na unazungumza tu maneno yanayosikika kuwa matamu ili Mungu asikie; nia zako mbalimbali za kijanja, huku, unajificha kutoka kwa Mungu, unajificha usionekane na Mungu, pamoja na maajabu, njama, na mipango yako, na unashikilia matarajio na hatima yako mikononi mwako, ukiwa na hofu kubwa kwamba huenda yakachukuliwa na Mungu. Hivyo, Mungu hatazamii uaminifu wa binadamu kwake Yeye. Ingawaje Mungu anaangalia kina cha moyo wa binadamu, na Anaweza kuona kile ambacho binadamu anafikiria na anataka kufanya moyoni mwake, na Anaweza kuona ni mambo yapi yamewekwa ndani ya moyo wake, moyo wa binadamu haumilikiwi na Mungu, hajautoa ili udhibitiwe na Mungu. Hivi ni kusema, Mungu anayo haki ya kuangalia, lakini Hana haki ya kuudhibiti moyo huo. Kwenye nadharia za kibinafsi za binadamu, binadamu hataki wala hanuii kujiacha kwenye huruma za Mwenyezi Mungu. Binadamu hajajifungia tu kutoka kwa Mungu, bali kuna hata watu wanaofikiria njia za kusetiri mioyo yao, kwa kutumia mazungumzo matamu na sifa za kinafiki ili kuunda hali ya uongo na kupata uaminifu wa Mungu, na kuficha uso wao wa kweli dhidi ya kuonekana na Mungu. Nia yao ya kutomruhusu Mungu kuona ni kutoruhusu Mungu kuelewa namna walivyo kwa kweli. Hawataki kutoa mioyo yao kwa Mungu lakini wanajihifadhi wao wenyewe. Maandishi madogo ya haya ni kwamba kile ambacho binadamu anafanya na kile ambacho anataka kimepangiliwa chote, kikapigiwa hesabu, na kuamuliwa na binadamu mwenyewe; haihitaji kushiriki au kuingilia kati kwa Mungu, na isitoshe hahitaji mipango na mipangilio ya Mungu. Hivyo, iwapo ni kuhusiana na amri za Mungu, agizo Lake, au mahitaji ambayo Mungu anamwekea binadamu, uamuzi wa binadamu unatokana na nia na maslahi yake mwenyewe, katika mazingira na hali yake mwenyewe ya wakati huo. Siku zote binadamu anatumia maarifa na maono ambayo amezoeana nayo, na akili zake binafsi ili kuamua na kuchagua njia anayofaa kutembelea na haruhusu uingiliaji kati au udhibiti wa Mungu. Huu ndio moyo wa binadamu ambao Mungu anaona.

Kuanzia mwanzo hadi leo, ni binadamu tu ambaye ameweza kuzungumza na Mungu. Yaani, miongoni mwa viumbe wote walio hai na viumbe wa Mungu, hakuna yeyote isipokuwa binadamu ameweza kuzungumza na Mungu. Binadamu anayo masikio yanayomwezesha kusikia, na macho yanayomwezesha kuona; anayo lugha na fikira zake binafsi, na pia anao uhuru wa kuamua chochote. Anamiliki kila kitu kinachohitajika kusikia Mungu akiongea, na kuelewa

mapenzi ya Mungu, na kukubali agizo la Mungu, na hivyo basi Mungu anayaweka matamania yake yote kwake binadamu, Akitaka kumfanya binadamu kuwa mwandani Wake ambaye anayo akili sawa na Yeye na ambaye anaweza kutembea na Yeye. Tangu Alipoanza kusimamia, Mungu amekuwa akisubiria binadamu kumpa moyo wake, kumwacha Mungu kuutakasa na kuufaa ipaswavyo, kumfanya yeye kumtosheleza Mungu na kupendwa na Mungu, kumfanya yeye kumstahi Mungu na kujiepusha na maovu. Mungu amewahi kutazamia mbele na kusubiria matokeo haya. Kunao watu kama hawa miongoni mwa rekodi za Biblia? Yaani, kunao wowote kwenye Biblia wanaoweza kutoa mioyo yao kwa Mungu? Kunaye yeyote anayetangulia kabla ya enzi hii? Leo, hebu tuendeleo kusoma simulizi za Biblia na kuangalia kama kile kilichofanywa na mhusika huyu—Ayubu—kina muunganisho wowote na mada ya “kumpa Mungu moyo wako” ambayo tunazungumzia kuhusu leo. Hebu tuone kama Ayubu alimtosheleza Mungu na kupendwa na Mungu.

Maoni yenu ni yapi kuhusu Ayubu? Wakitolea mifano ya maandiko asilia, baadhi ya watu husema kwamba Ayubu “alimcha Mungu na kujiepusha na maovu.” “Alimcha Mungu na kujiepusha na maovu”: Huo ndio ukadiriaji mojawapo asilia wa Ayubu uliorekodiwa kwenye Biblia. Kama mliyatumia maneno yenu binafsi, mnawezaje kumzungumzia Ayubu? Baadhi ya watu wanasema kwamba Ayubu alikuwa binadamu mzuri mwenye busara, baadhi wanasema kwamba alikuwa na imani ya kweli kwa Mungu; baadhi wanasema kwamba Ayubu alikuwa binadamu mwenye haki na utu. Mmeiona imani ya Ayubu, hivi ni kusema, katika mioyo yenu mnaambatisha umuhimu mkubwa kwa na mnaonea wivu imani ya Ayubu. Leo, basi, hebu tuzungumzie kile kilichomilikiwa na Ayubu ambacho Mungu anafurahishwa sana naye. Kisha, hebu tusome maandiko yaliyo hapa chini.

C. Ayubu

1. Ukadiriaji wa Ayubu na Mungu na kwenye Biblia

Ayubu 1:1 Kulikuwa na mtu katika nchi ya Uzi, ambaye alitwa Ayubu; na huyo mtu alikuwa mtimilifu na mwaminifu, na ambaye alimcha Mungu, na kuepuka maovu.

Ayubu 1:5 Na ilikuwa hivyo, wakati hizo siku zao za karamu ziliisha, Ayubu aliwatuma na kuwatakasa, na akaamka asubuhi mapema, na kutoa sadaka za kuteketezwa kulingana na hesabu yao wote; kwa sababu Ayubu alisema, Inaweza kuwa kwamba wana wangu wametenda dhambi, na kumlaani Mungu mioyoni mwao. Hivyo ndivyo Ayubu alivyofanya kila siku.

Ayubu 1:8 Naye Yehova akasema kwa Shetani, je, umemfikiria mtumishi Wangu Ayubu, kwamba hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu?

Ni nini hoja kuu unayoiona kwenye vifungu hivi? Vifungu hivi vitatu vifupi vya maandiko vyote vinahusu Ayubu. Ingawaje ni vifupi, vinaelezea waziwazi alikuwa mtu wa aina gani. Kupitia kwa ufafanuzi wake kuhusu tabia ya kila siku ya Ayubu na mwenendo wake, vinaelezea kila mmoja kwamba, badala ya kukosa msingi, ukadiriaji wa Mungu ya Ayubu ulikuwa na msingi wake na ulikuwa umekita mizizi. Vinatambia kwamba, iwapo ni utathmini wa binadamu kuhusu Ayubu (Ayubu 1:1), au utathmini wa Mungu kuhusu yeye (Ayubu 1:8), tathmini zote zinatokana na matendo ya Ayubu mbele ya Mungu na binadamu (Ayubu 1:5).

Kwanza, hebu tukisome kifungu nambari moja: “Kulikuwa na mtu katika nchi ya Uzi, ambaye aliitwa Ayubu; na huyo mtu alikuwa mtimilifu na mwaminifu, na ambaye alimcha Mungu, na kuepuka maovu.” Ukadiriaji wa kwanza wa Ayubu kwenye Biblia, sentensi hii ndiyo utathmini wa mwandishi kuhusu Ayubu Kiasili, unawakilisha pia ukadiriaji wa binadamu kuhusu Ayubu, ambayo ni “huyo mtu alikuwa mtimilifu na mwaminifu, na ambaye alimcha Mungu, na kuepuka maovu.” Kisha, hebu tuusome utathmini wa Mungu kuhusu Ayubu: “Hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu” (Ayubu 1:8). Kati ya tathmini hizi mbili, moja ilitoka kwa binadamu, na nyingine ikatoka kwa Mungu; ni ukadiriaji aina mbili ulio na maudhui moja. Inaweza kuonekana, basi, kwamba tabia na mwenendo wa Ayubu ulijulikana kwa binadamu, na pia ulisifiwa na Mungu. Kwa maneno mengine, mwenendo wa Ayubu mbele ya binadamu na mwenendo wake mbele ya Mungu ulikuwa sawa; aliweka tabia yake na motisha yake mbele ya Mungu siku zote, ili hivi viwili viweze kuangaliwa na Mungu, na yeye alikuwa mmoja aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu. Hivyo, katika macho ya Mungu, kati ya watu duniani, ni Ayubu tu ambaye alikuwa mtimilifu na mnyofu, ndiye aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu.

Maonyesho Mahususi ya Kumcha Mungu kwa Ayubu na Kujiepusha na Maovu katika Maisha Yake ya Kila siku

Kisha, hebu tuangalie maonyesho mahususi ya kumcha Mungu kujiepusha na maovu kwa Ayubu. Juu ya vifungu hivi vinavyotangulia na kufuata, hebu pia tusome Ayubu 1:5, ambayo ni mojawapo ya maonyesho mahususi ya kumcha Mungu na kujiepusha kwa maovu kwa Ayubu. Inahusu namna ambavyo alimcha Mungu na kujiepusha na maovu katika maisha yake ya kila siku; muhimu zaidi, hakufanya tu kile alichostahili kufanya kwa minajili ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu kwake, lakini pia mara kwa mara alitoa sadaka iliyoteketezwa mbele ya Mungu kwa niaba ya wana wake. Alikuwa na hofu kwamba walikuwa mara nyingi “wametenda dhambi, na kumlaani Mungu katika mioyo yao” wakati wakiwa na karamu. Na uoga huu ulijionyesha vipi ndani ya Ayubu? Maandishi asilia yanatupa simulizi ifuatayo: “Na ilikuwa hivyo, wakati hizo siku zao za karamu ziliisha, Ayubu aliwatuma na kuwatakasa, na akaamka

asubuhi mapema, na kutoa sadaka za kuteketezwa kulingana na hesabu yao wote.” Mwenendo wa Ayubu unatuonyesha kwamba, badala ya kuonyeshwa katika tabia yake ya nje, kumcha Mungu kwake kulitokea ndani ya moyo wake, na kwamba kumcha Mungu kwake kungepatikana katika kila kipengele cha maisha yake ya kila siku, wakati wote, kwani hakujipusha na maovu tu yeye mwenyewe, lakini pia alitoa sadaka zilizoteketezwa kwa niaba ya watoto wake wa kiume. Kwa maneno mengine, Ayubu hakuwa tu mwenye hofu ya kutenda dhambi dhidi ya Mungu na kumkataa Mungu katika moyo wake, lakini pia alikuwa na wasiwasi kwamba watoto wake wa kiume walitenda dhambi dhidi ya Mungu na kumkataa Yeye katika moyo yao. Kutokana na haya ukweli unaweza kuonekana kwamba ukweli wa kumcha Mungu kwa Ayubu unapita uchunguzi, na ni zaidi ya shaka ya binadamu yeyote. Je, alifanya hivi mara kwa mara, au mara nyingi? Sentensi ya mwisho ya maandishi ni “Hivyo ndivyo Ayubu alivyofanya kila siku.” Maana ya maneno haya ni kwamba Ayubu hakuenda na kuangalia watoto wake mara kwa mara au wakati alipenda kufanya hivyo, wala hakutubu kwa Mungu kupitia kwa maombi. Badala yake, aliwatumia mara kwa mara na kuwatakaswa watoto wake wa kiume kutoa sadaka iliyoteketezwa kwa niaba yao. Hiyo kauli “bila kusita” hapa haimaanishi alifanya hivyo kwa siku moja au mbili, au kwa muda mfupi tu. Inasema kwamba maonyesho ya kumcha Mungu kwa Ayubu hayakuwa ya muda, na hayakusita kwa maarifa aliyokuwa nayo au kwa maneno aliyotamka; badala yake, njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu iliongoza moyo wake, iliamuru tabia yake, na ilikuwa, ndani ya moyo wake mzizi wa uwepo wake. Kwamba alifanya hivyo bila kusita yaonyesha kwamba, katika moyo wake, mara nyingi alikuwa na hofu kwamba yeye mwenyewe angetenda dhambi dhidi ya Mungu na alikuwa na wasiwasi pia kwamba watoto wake wa kiume na binti zake walitenda dhambi dhidi ya Mungu. Inawakilisha namna tu ambavyo uzito wa njia ambayo alimcha Mungu na kujiepusha na maovu ulibebwa ndani ya moyo wake. Alifanya hivyo bila kusita kwa sababu, ndani ya moyo wake, alikuwa na hofu na wasiwasi—wasiwasi kwamba alikuwa ametenda maovu na kutenda dhambi dhidi ya Mungu, na kwamba alikuwa amepotoka kutoka kwenye njia ya Mungu, na basi alikuwa hawezi kutosheleza Mungu. Wakati huohuo, alikuwa pia na wasiwasi kuhusu watoto wake wa kiume na binti zake, akiogopa kwamba walikuwa wamemkosea Mungu. Hivyo ndivyo ulivyokuwa mwenendo wa kawaida wa Ayubu katika maisha yake ya kila siku. Kwa hakika ni mwenendo wa kawaida ambao unathibitisha kwamba kumcha Mungu na kujiepusha kwa maovu kwa Ayubu si maneno matupu tu, kwamba Ayubu aliishi kwa kudhihirisha kwa kweli ukweli kama huo. “Hivyo ndivyo Ayubu alivyofanya kila siku”: Maneno haya yanatuambia kuhusu matendo ya kila siku ya Ayubu mbele ya Mungu. Alipofanya hivi bila kusita, tabia yake na moyo wake vilifika mbele ya Mungu? Kwa maneno mengine, Mungu mara nyingi alipendezwa na moyo wake na tabia yake? Basi, ni katika hali gani na katika muktadha gani Ayubu alifanya hivi bila kusita? Baadhi ya watu wanasema kwamba ilikuwa ni kwa sababu Mungu alijitokeza kwa Ayubu mara kwa mara

na ndiyo maana akatenda hivi; baadhi wanasema kwamba alifanya hivi bila kusita kwa sababu angejipusha na maovu; na baadhi wanasema kwamba alifikiria kwamba utajiri wake ulikuwa haujaja kwa urahisi, na alijua kwamba alikuwa amepewa na Mungu, na hivyo alikuwa na uoga mwingi wa kupoteza mali yake kutokana na kutenda dhambi dhidi ya au kumkosea Mungu. Je, yapo madai yoyote kati ya haya yaliyo kweli? Bila shaka la. Kwani, kwa macho ya Mungu, kile Mungu amekubali na kupenda sana kuhusu Ayubu si tu kwamba alifanya hivi bila kusita; zaidi ya hapo, ilikuwa ni mwenendo wake mbele ya Mungu, binadamu, na Shetani alipokabidhiwa Shetani na kujaribiwa. Sehemu zilizo hapa chini zinatupa ithibati yenye ushawishi mkubwa zaidi, ithibati ambayo inatuonyesha ukweli wa ukadiriaji wa Mungu kwa Ayubu. Kinachofuata, hebu tusome maandiko kwenye vifungu vifuatavyo.

2. Shetani Anamjaribu Ayubu kwa Mara ya Kwanza (Mifugo Yake Yaibiwa na Janga Lawapata Watoto Wake)

a. Maneno Yaliyotamkwa na Mungu

Ayubu 1:8 Naye Yehova akasema kwa Shetani, je, umemfikiria mtumishi Wangu Ayubu, kwamba hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu?

Ayubu 1:12 Naye Yehova akasema kwa Shetani, Tazama, vyote ambavyo anavyo vimo uwezoni mwako; lakini juu yake mwenyewe wewe usinyoshe mkono wako. Hivyo basi Shetani akaondoka mbele za uwepo wa Yehova.

b. Jibu la Shetani

Ayubu 1:9-11 Kisha Shetani akamjibu Yehova, na kusema, je, Ayubu anamcha Mungu bure? Wewe hujamzunguka kila upande na ukingo, na kila upande wa nyumba yake, na kila upande wa yote aliyo nayo? Umebariki kazi ya mikono yake, na mali yake inaongezeka nchini. Lakini nyosha mbele mkono Wako sasa, na uguse yote aliyo nayo, na yeye atakulaani mbele ya uso Wako.

Mungu Amruhusu Shetani Kumjaribu Ayubu ili Imani ya Ayubu iweze Kufanywa Kuwa Timilifu

Ayubu 1:8 ndiyo rekodi ya kwanza tunayoiona kwenye Biblia kuhusu mabadilishano kati ya Yehova Mungu na Shetani. Na ni nini alichosema Mungu? Maandishi asilia yanatupatia simulizi ifuatayo: “Naye Yehova akasema kwa Shetani, je, umemfikiria mtumishi Wangu Ayubu, kwamba hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu?” Huu ulikuwa ukadiriaji wa Mungu kuhusu Ayubu kwa Shetani;

Mungu alisema kwamba alikuwa binadamu mtimilifu na mnyofu, yule aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu. Kabla ya maneno haya kati ya Mungu na Shetani, Mungu alikuwa ameamua kwamba Angemtumia Shetani kujaribu Ayubu—kwamba Angemkabidhi Ayubu kwa Shetani. Kwa mkondo mmoja, hali hii ingethibitisha kwamba uangalizi na utathmini wa Mungu kwa Ayubu ulikuwa sahihi na bila kosa, na ungesababisha Shetani kuaibishwa kupitia kwa ushuhuda wa Ayubu, kwa mkondo mwingine, ingefanya imani ya Ayubu kwa Mungu na kumcha Mungu kuwa timilifu. Hivyo, wakati Shetani alipokuja mbele ya Mungu, Mungu hakutatiza maneno. Alienda moja kwa moja kwenye hoja na kumuuliza Shetani: “Je, umemfikiria mtumishi Wangu Ayubu, kwamba hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu?” Katika swali la Mungu kunayo maana ifuatayo: Mungu alijua kwamba Shetani alizunguka kila pahali, na mara nyingi alikuwa amemnyemelea Ayubu, aliyekuwa mtumishi wa Mungu. Alikuwa mara nyingi amemjaribu na kumshambulia, akijaribu kupata njia ya kumwangamiza Ayubu ili kuthibitisha kwamba imani ya Ayubu katika Mungu na kumcha Mungu kwake kusingeweza kubadilika. Shetani pia alitafuta kwa haraka sana fursa za kumhangaisha Ayubu, ili Ayubu aweze kumkataa Mungu, na kwamba aweze kumpokonya kutoka katika mikono ya Mungu. Lakini Mungu aliuangalia moyo wa Ayubu na kuona kwamba alikuwa mtimilifu na mnyofu, na kwamba alimcha Mungu na kujiepusha na maovu. Mungu alitumia swali moja kumwambia Shetani kwamba Ayubu alikuwa binadamu mtimilifu na mnyofu aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu, kwamba Ayubu asingeweza kumwacha Mungu na kufuata Shetani. Baada ya kusikia utathmini wa Mungu kuhusu Ayubu, ndani ya Shetani kukatokea hasira kali iliyotokana na udhalilishaji, na akawa mwenye hasira zaidi, na aliyekosa subira ya kumpokonya Ayubu kutoka kwa Mungu, kwani Shetani alikuwa hajawahi kusadiki kwamba mtu angeweza kuwa mtimilifu na mnyofu, au kwamba angeweza kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Wakati huohuo, Shetani pia alichukizwa na utimilifu na unyofu kwa binadamu, na aliwachukia watu ambao wangeweza kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Na hivyo imeandikwa katika Ayubu 1:9-11 kwamba “Kisha Shetani akamjibu Yehova, na kusema, je, Ayubu anamcha Mungu bure? Wewe hujamzunguka kila upande na ukingo, na kila upande wa nyumba yake, na kila upande wa yote aliyo nayo? Umebariki kazi ya mikono yake, na mali yake inaongezeka nchini. Lakini nyosha mbele mkono Wako sasa, na uguse yote aliyo nayo, na yeye atakulaani mbele ya uso Wako.” Mungu alikuwa amezoea kwa undani asili ya kijicho ya Shetani, na Alijua vizuri kabisa kwamba Shetani alikuwa na mpango wa muda mrefu wa kumwangamiza Ayubu, na hivyo kwa haya Mungu alitaka, kwa kumwambia Shetani kwa mara nyingine kwamba Ayubu alikuwa mtimilifu na mnyofu na kwamba alimwogopa Mungu na kujiepusha na maovu, kumrudisha Shetani pale anapofaa, kumfanya Shetani kufichua uso wake wa kweli na kumshambulia na kumjaribu Ayubu. Kwa maneno mengine, Mungu alitilia mkazo makusudi kwamba Ayubu alikuwa mtimilifu na mnyofu

na kwamba alimcha Mungu na kujiepusha na maovu, na kwa njia hii alimfanya Shetani kumshambulia Ayubu kwa sababu ya chuki na hasira za Shetani kutokana na vile ambavyo Ayubu alikuwa binadamu mtimilifu na mnyofu, yule aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu. Kutokana na haya, Mungu angemletea Shetani aibu kupitia kwa ukweli kwamba Ayubu alikuwa binadamu mtimilifu na mnyofu, yule aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu, na Shetani angeachwa akiwa amedhalilishwa kabisa na kushindwa. Baada ya hapo, Shetani asingekuwa tena na shaka au asingetoa mashtaka kuhusu utimilifu, unyofu, ucha Mungu au hali ya kujiepusha na maovu ya Ayubu. Kwa njia hii, majaribio ya Mungu na yale ya Shetani yalikuwa karibu yasiyoepukika. Yule tu aliye na uwezo wa kustahimili majaribio ya Mungu na yale ya Shetani alikuwa ni Ayubu. Kufuatia mabadilishano haya, Shetani alipewa ruhusa kumjaribu Ayubu. Na hivyo raundi ya kwanza ya mashambulizi ya Shetani ikaanza. Kilengwa cha mashambulizi haya kilikuwa mali ya Ayubu, kwani Shetani alikuwa ametoa mashtaka yafuatayo dhidi ya Ayubu: “Je, Ayubu anamcha Mungu bure? ... Umebariki kazi ya mikono yake, na mali yake inaongezeka nchini.” Kutokana na haya, Mungu alimruhusu Shetani kuchukua kila kitu ambacho Ayubu alikuwa nacho—ambalo ndilo lilikuwa kusudio lenyewe la Mungu kuzungumza na Shetani. Hata hivyo, Mungu alitoa sharti moja kwa Shetani: “Vyote ambavyo anavyo vimo uwezoni mwako; lakini juu yake mwenyewe wewe usinyoshe mkono wako” (Ayubu 1:12). Hili ndilo sharti ambalo Mungu alitoa baada ya kumruhusu Shetani kumjaribu Ayubu na akamweka Ayubu kwenye mikono ya Shetani, na hiyo ndiyo mipaka aliyomwekea Shetani: Alimwamuru Shetani kutodhuru Ayubu. Kwa sababu Mungu alijua kwamba Ayubu alikuwa mtimilifu na mnyofu, na kwamba Alikuwa na imani kwamba utimilifu na unyofu wa Ayubu kwake Yeye ulikuwa zaidi ya kutiliwa shaka, na kwamba angeweza kustahimili majaribio; hivyo, Mungu alimruhusu Shetani kumjaribu Ayubu, lakini akaweka hapo kizuizi kwa Shetani: Shetani aliruhusiwa kuchukua mali ya Ayubu yote, lakini asimguse hata kwa kidole. Hii inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba Mungu hakumkabidhi Ayubu kabisa kwa Shetani wakati huo. Shetani angeweza kumjaribu Ayubu kwa mbinu zozote zile ambazo alitaka, lakini hakuweza kumdhuru Ayubu mwenyewe, hata unywele mmoja wa kichwa chake, kwa sababu kila kitu cha binadamu kinathibitiwa na Mungu, iwapo binadamu anaishi ama anakufa inaamuliwa na Mungu na Shetani hana leseni yoyote ya kuthibiti haya. Baada ya Mungu kumwambia Shetani maneno haya, Shetani asingeweza kusubiri kuanza. Alitumia kila mbinu kumjaribu Ayubu, na baada ya muda usiyokuwa mrefu Ayubu alipoteza kundi kubwa la kondoo na ng’ombe na mali yote aliyokuwa amepewa na Mungu.... Na hivyo majaribio ya Mungu yakamjia yeye.

Ingawa Biblia inatuambia asili ya jaribio la Ayubu, je Ayubu mwenyewe, ambaye alipatwa na majaribio haya, alijua kuhusu kile kilichokuwa kikiendelea? Ayubu alikuwa tu binadamu wa kawaida; bila shaka hakujua chochote kuhusu hadithi ile iliyokuwa ikiendelea nyuma yake. Hata

hivyo, kumcha Mungu kwake na utimilifu pamoja na unyofu wake, ulimfanya kutambua kwamba majaribio ya Mungu yalikuwa yamemjia. Hakujua ni nini kilichokuwa kimefanyika kwenye ufalme wa kiroho, wala nia alizokuwa nazo Mungu katika majaribio hayo. Lakini alijua kwamba haijalishi ni nini ambacho kingemfanyikia yeye, alifaa kuendelea kushikilia ukweli wa utimilifu na unyofu wake, na kwamba alifaa kutii njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Mwelekeo na mwitikio wa Ayubu katika masuala haya uliweza kutazamwa waziwazi na Mungu. Naye Mungu aliona nini? Aliuona moyo wa Ayubu uliyomcha Mungu, kwa sababu kutoka mwanzo hadi wakati ambapo Ayubu alijaribiwa, moyo wa Ayubu ulibakia wazi kwa Mungu, uliwekwa mbele ya Mungu, naye Ayubu hakuwacha utimilifu wala unyofu wake, wala hakutupilia mbali au kugeuka katika njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu—na hakuna kingine chochote kilichokuwa cha kumtosheleza na kumfurahisha Mungu kama haya. Kisha, tutaangalia ni majaribio yapi aliyoyapitia Ayubu na ni vipi ambavyo aliyashughulikia majaribio haya. Hebu tuyasome maandiko.

c. Mwitikio wa Ayubu

Ayubu 1:20-21 Kutoka hapo Ayubu akainuka, na akalipasua joho lake, na akanyoa kichwa chake, na akaanguka chini, na kuabudu, Naye akasema, Nilitoka kwa tumbo la mama yangu nikiwa uchi, na mimi nitarudi huko nikiwa uchi; Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe.

Kwamba Ayubu Anajiwajibikia Yeye Mwenyewe Kurudisha Vyote Anavyomiliki Kunatokana na Kumcha Kwake Mungu

Baada ya Mungu kumwambia Shetani, “Vyote ambavyo anavyo vimo uwezoni mwako; lakini juu yake mwenyewe wewe usinyoshe mkono wako.” Shetani aliondoka, muda mfupi baadaye Ayubu alipata mashambulizi ya ghafla na makali: Kwanza, ng’ombe na punda wake waliibwa na watumishi wake kuuwawa; kisha, kondoo na watumishi wake waliteketezwa hadi kiwango cha kuangamia; baada ya hapo ngamia wake walichukuliwa na watumishi wake wakauliwa; hatimaye watoto wake wa kiume na wa kike waliaga dunia. Msururu huu wa mashambulizi ulikuwa ni mateso ambayo alipitia Ayubu kwenye jaribio hili la kwanza. Kama alivyoamrishwa na Mungu, kwenye kipindi hiki cha mashambulizi, Shetani alilenga tu mali ya Ayubu na watoto wake, na hakumdhuru Ayubu mwenyewe. Hata hivyo, Ayubu alibadilishwa papo hapo kutoka kuwa mtu tajiri aliyemiliki utajiri mwingi hadi kuwa mtu asiye na chochote wala lolote. Hakuna yeyote ambaye angestahimili mshangao huu mkubwa au ambaye angeitikia vizuri, ilhali Ayubu aliuonyesha upande wake usio wa kawaida. Maandiko yanaelezea yafuatayo: “Kutoka hapo Ayubu akainuka, na akalipasua joho lake, na akanyoa kichwa chake, na akaanguka chini, na kuabudu.” Huu ndio uliokuwa mwitikio wa kwanza wa Ayubu baada ya kusikia

kwamba watoto wake walikuwa wameaga dunia na alikuwa amepoteza mali yake yote. Zaidi ya yote, hakuonekana ni kana kwamba ameshangazwa, au amepigwa na butwaa chakari, isitoshe hakuonyesha hasira au chuki. Unaona, basi, kwamba moyoni mwake alikuwa tayari ametambua kuwa majanga haya hayakuwa ajali, au yalitokana na mkono wa binadamu, na wala hayakuwa kuwasili kwa kuadhibiwa au adhabu. Badala yake, majaribio ya Yehova yalikuwa yamemjia yeye; alikuwa ni Yehova ambaye alitaka kuchukua mali na watoto wake. Ayubu alikuwa mtulivu na mwenye kuelewa haraka wakati huo. Ubinadamu wake wa utimilifu na unyofu ulimwezesha yeye kuweza kufanya uamuzi na uamuzi kwa usahihi kwa njia ya kiasili na kirazini hasa, kuhusu majanga yaliyokuwa yamemsibu, na matokeo yake ni kuwa, alijiendeleza kwa utulivu usio wa kawaida. “Kutoka hapo Ayubu akainuka, na akalipasua joho lake, na akanyoa kichwa chake, na akaanguka chini, na kuabudu.” “Akalipasua joho lake” inamaanisha kwamba alikuwa hana nguo, na hakumiliki chochote; “akanyoa kichwa chake” inamaanishwa kwamba alikuwa amerudi mbele ya Mungu kama mtoto mchanga aliyezaliwa; “akaanguka chini, na kuabudu” inamaanisha alikuwa amekuja ulimwenguni akiwa uchi, na bado hakuwa na chochote leo, alirudishwa kwa Mungu kama mtoto mchanga aliyezaliwa. Mwelekeo wa Ayubu kwa yote yaliyompata usingeweza kutimizwa na kiumbe yeyote wa Mungu. Imani yake kwa Yehova ilizidi ile ufalme wa imani; huku kulikuwa ni kumcha Mungu kwake, kuwa mtiifu kwa Mungu, na hakuweza tu kutoa shukrani kwa Mungu kwa kumpa yeye lakini pia kuchukua kutoka kwake. Na zaidi ya hayo, aliweza kujiwajibikia yeye mwenyewe ili kurudisha yale yote aliyomiliki, pamoja na maisha yake.

Kumcha Mungu na utiifu wa Ayubu kwa Mungu ni mfano kwa wanadamu, na utimilifu na unyofu wake ulikuwa ndio kilele cha ubinadamu unaofaa kumilikiwa na binadamu. Ingawaje hakumwona Mungu, alitambua kwamba Mungu kwa kweli alikuwepo, na kwa sababu ya utambuzi huu alimcha Mungu, na kutokana na kumcha Mungu kwake, aliweza kumtii Mungu. Alimpa Mungu uhuru wa kuchukua chochote alichokuwa nacho, ilhali hakulalamika, na akaanguka chini mbele ya Mungu na kumwambia kwamba kwa wakati huohuo, hata kama Mungu angeuchukua mwili wake, angemruhusu yeye kufanya hivyo kwa furaha, bila malalamiko. Mwenendo wake wote ulitokana na ubinadamu wake timilifu na mnyofu. Hivi ni kusema, kutokana na kutokuwa na hatia kwake, uaminifu, na upole wake, Ayubu hakutikisika katika utambuzi wake na uzoefu wa uwepo wa Mungu na juu ya msingi huu aliweza kujitolea madai yeye mwenyewe na kuwastanisha kufikiria kwake, tabia, mwenendo, na kanuni za vitendo mbele ya Mungu kulingana na mwongozo wa Mungu kwake yeye na vitendo vya Mungu ambavyo alikuwa ameviona miongoni mwa mambo mengine yote. Baada ya muda, uzoefu wake ulimsababisha yeye kuwa na hali halisi na ya kweli ya kumcha Mungu na kumfanya pia kujiepusha na maovu. Hiki ndicho kilikuwa chanzo cha uadilifu ambao Ayubu alishikilia. Ayubu

aliumiliki ubinadamu wa uaminifu, usio na hatia, na wa upole, na alikuwa na uzoefu halisi wa kumcha Mungu, kumtii Mungu na kujiepusha na maovu, pamoja na maarifa kwamba “Yehova alinipa, na Yehova amechukua.” Ni kwa sababu tu ya mambo haya ndiyo aliweza kusimama imara na kushuhudia katikati ya mashambulizi mabaya kama yale yaliyomsibu kutoka kwa Shetani, na ni kwa sababu tu ya hayo ndiyo aliweza kutomkasirisha Mungu na kutoa jibu la kutosheleza kwake Mungu wakati majaribio ya Mungu yalipomjia. Ingawaje mwenendo wa Ayubu kwenye jaribio la kwanza ulikuwa wa moja kwa moja, vizazi vya baadaye havikuwa na uhakika wa kutimiza hali hiyo ya moja kwa moja hata baada ya kutia bidii maisha yao yote, wala hawangemiliki kwa vyovyote vile mwenendo wa Ayubu uliofafanuliwa hapo juu. Leo, wakikabiliwa na mwenendo wa moja kwa moja wa Ayubu, na katika kuulinganisha na kilio na bidii ya “utiifu wenye hakika na uaminifu hadi kifo” ulioonyeshwa kwa Mungu na wale wanaodai kusadiki Mungu na kufuata Mungu, je mnahisi aibu kwa kina au la?

Wakati unasoma maandiko kuhusu yale mateso yote aliyopitia Ayubu na familia yake, mwikio wako ni upi? Unapotea kwenye fikira zako? Unashangazwa? Je, majaribio haya yaliyomsibu Ayubu yanaweza kufafanuliwa kama ya “kusikitisha”? Kwa maneno mengine, inatisha vya kutosha kuyasoma majaribio ya Ayubu kama yalivyofafanuliwa kwenye maandiko, kutosema chochote kuhusu vile yangukuwa katika uhalisia. Unaona, basi, kwamba kile kilichomsibu Ayubu hakikuwa “mazoezi,” lakini “vita,” halisi vikiwa na “bunduki” na “risasi” za kweli. Lakini nani alisababisha yeye kuweza kupitia majaribio haya? Yaliweza, bila shaka, kutekelezwa na Shetani, yalitekelezwa na Shetani mwenyewe—lakini yalidhinishwa na Mungu. Je, Mungu alimwambia Shetani kumjaribu Ayubu kwa njia gani? Hakumwambia. Mungu alimpa Shetani sharti moja tu, na baadaye jaribio hilo likamjia Ayubu. Wakati jaribio lilimjia Ayubu, liliwapatia watu hisia ya maovu na ubaya wa Shetani, ya uoneaji kijicho wake, na uchukivu wake kwa binadamu, na uadui wake kwa Mungu. Katika haya tunaona kwamba maneno yasingeweza kufafanua namna tu ambavyo jaribio hili lilikuwa la kikatili. Inaweza kusemekana kwamba asili ya kijicho ambayo Shetani alimnyanyasa binadamu, na uso wake mbaya, vyote vilichuliwa kabisa kwa wakati huu. Shetani alitumia fursa hii, fursa iliyotolewa kupitia kwa ruhusa ya Mungu, kumnyanyasa Ayubu kwa njia mbaya na ya kusikitisha, mbinu na kiwango cha ukatili ambao haufikiriki na hauvumiliki kabisa na watu wa leo. Badala ya kusema kwamba Ayubu alijaribiwa na Shetani, na kwamba alisimama imara katika ushuhuda wake wakati wa jaribio hili, ni bora zaidi kusema kwamba katika majaribio hayo yaliyokuwa mbele yake kutoka kwa Mungu, Ayubu alianza kuwa katika mapambano na Shetani ili kuulinda utimilifu na unyofu wake, kutetea njia yake ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Katika shindano hili, Ayubu alipoteza kundi kubwa la kondoo na ng’ombe, alipoteza mali yake yote na watoto wake wa kike na kiume—lakini hakuacha utimilifu, unyofu, au hali yake ya kumcha Mungu. Kwa maneno

mengine, katika pigano hili na Shetani alipendelea kunyang'anywa mali na watoto kuliko kupoteza utimilifu, unyofu na hali yake ya kumcha Mungu. Alipendelea kushikilia mzizi wa maana ya kuwa binadamu. Maandiko yanatoa simulizi halisi kuhusu mchakato wote ambao Ayubu alipoteza rasilimali zake, na pia ukasimulia mwenendo na mwelekeo wa Ayubu. Simulizi hizi za mkato, na wazi zinatoa hisia kwamba Ayubu alikuwa karibu anao utulivu wakati akipitia jaribio hili, lakini kama kile kilichofanyika kwa hakika kingeundwa upya, na kuongeza asili yale ya kijicho ya Shetani—basi mambo yasingekuwa rahisi au mepesi kama yalivyofafanuliwa kwenye sentensi hizi. Uhalisia ulikuwa wenye ukatili zaidi. Hicho ndicho kiwango cha uharibifu na chuki ambacho Shetani hushughulikia wanadamu na wale wote wanaoidhinishwa na Mungu. Kama Mungu asingekuwa amemwomba Shetani kutodhuru Ayubu, Shetani bila shaka angekuwa amemwua bila ya shaka. Shetani hataki mtu yeyote kumwabudu Mungu, wala hataki wale wenye haki mbele ya macho ya Mungu na wale walio timilifu na wanyofu kuweza kuendelea kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Kwa watu kumcha Mungu na kujiepusha maovu kunamaanisha kwamba wanajiepusha na kumwacha Shetani, na hivyo Shetani alitumia ruhusa ya Mungu kumlimbikizia hasira yake na chuki kwake Ayubu bila huruma. Unaona, basi, mateso aliyoyapitia Ayubu yalikuwa mengi sana, haya yalikuwa mengi kiasi gani ambayo Ayubu alipitia, kuanzia kwenye akili hadi kwenye mwili, kutoka nje hadi ndani. Leo, hatuoni namna ambavyo kwa wakati huu na tunaweza tu kupata kutoka kwenye simulizi za Biblia, mtazamo mfupi wa hisia za Ayubu wakati alipokuwa akipitia yale mateso wakati huo.

Kutotikisika kwa Uadilifu wa Ayubu Kunaleta Aibu Kwake Shetani na Kusababisha Shetani Kutoroka kwa Wasiwasi

Na ni nini ambacho Mungu alifanya wakati Ayubu alipopitia mateso haya? Mungu aliangalia, na kutazama, na Akasubiri matokeo. Wakati Mungu Alipokuwa akiangalia na kutazama, Alihisi vipi? Alihisi kuwa mwenye huzuni, bila shaka. Lakini, kutokana na huzuni Yake, Aliweza kujuta ruhusa Yake kwa Shetani ya kumjaribu Ayubu? Jibu ni, La, Asingefanya hivyo. Kwani Yeye alisadiki kwa dhati kwamba Ayubu alikuwa mtimilifu na mnyofu, kwamba alimcha Mungu na kujiepusha na maovu. Mungu alikuwa amempa Shetani tu fursa ya kuthibitisha uhaki wa Ayubu mbele ya Mungu, na kufichua maovu yake Shetani na hali ya kudharauliwa kwake binafsi. Ilikuwa, zaidi ya hapo, fursa ya Ayubu kutolea ushuhuda utakatifu wake na kumcha Mungu kwake na kujiepusha na maovu mbele ya watu wa ulimwengu, Shetani, na hata wale wanaomfuata Mungu. Je, matokeo ya mwisho yalithibitisha kwamba ukadiriaji wa Mungu kuhusu Ayubu ulikuwa sahihi na bila makosa? Je, Ayubu alimshinda kweli Shetani? Hapa tunasoma kuyahusu maneno yale halisi yaliyozungumzwa na Ayubu, maneno ambayo ni thibitisho kwamba alikuwa amemshinda Shetani. Alisema: “Nilitoka kwa tumbo la mama yangu nikiwa uchi, na mimi nitarudi huko nikiwa uchi.” Huu ndio mwelekeo wa utiifu ambao Ayubu

anao kwa Mungu. Kisha, akasema: “Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe.” Maneno haya yaliyozungumzwa na Ayubu yanathibitisha kwamba Mungu anaangalia kina cha moyo wa binadamu, kwamba Anaweza kuangalia kwenye akili ya binadamu, na yanathibitisha kwamba kuidhinisha kwake kwa Ayubu hakuna kosa, kwamba binadamu huyu aliyeidhinishwa na Mungu alikuwa mwenye haki. “Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe.” Maneno haya ni ushuhuda wa Ayubu kwa Mungu. Yalikuwa maneno haya ya kawaida yaliyomfanya Shetani kuogopa, yaliyoleta aibu kwake na kumsababisha kutoroka kwa wasiwasi, na, vilevile, yaliyomfunga pingu Shetani na kumuacha bila rasilimali zozote. Hivyo, pia, ndivyo maneno haya yalivyomfanya Shetani kuhisi matendo ya kustaajabisha na yenye nguvu ya Yehova Mungu, na kumruhusu kuelewa haiba kubwa na isiyo ya kawaida ya yule ambaye moyo wake ulitawaliwa na njia ya Mungu. Zaidi, yalionyesha Shetani nguvu za kipekee zilizoonyeshwa na mtu mdogo asiyekuwa na umuhimu wowote katika kutii njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu Shetani hivyo basi alishindwa kwenye shindano la kwanza. Licha ya utambuzi wake “uliopatikana kwa hali ngumu,” Shetani hakuwa na nia ya kumwachilia Ayubu, wala hakukuwa na badiliko lolote katika asili yake ya unafiki. Shetani alijaribu kuendelea kumshambulia Ayubu, na kwa mara nyingine tena akamjia Mungu ...

Kisha, hebu tuyasome maandiko kuhusu mara ya pili ambapo Ayubu alijaribiwa.

3. Shetani Amjaribu Ayubu Mara Nyingine Tena (Majipu Mabaya Yaupiga Mwili wa Ayubu)

a. Maneno Yaliyotamkwa na Mungu

Ayubu 2:3 Naye Yehova akasema kwa Shetani, je, umemfikiria mtumishi Wangu Ayubu, kwamba hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu? Na bado anashikilia ukamilifu wake, ingawa ulinichochea dhidi yake, ili mimi nimwangamize bila sababu.

Ayubu 2:6 Naye Yehova akasema kwa Shetani, Tazama, yeye yuko katika mkono wako; lakini uuhifadhi uhai wake.

b. Maneno Yaliyotamkwa na Shetani

Ayubu 2:4-5 Naye Shetani akamjibu Yehova, na akasema, Ngozi kwa ngozi, ndiyo, yote ambayo mtu anayo atayatoa kwa sababu ya uhai wake. Lakini nyosha mbele mkono Wako sasa, na uguse mfupa wake na nyama yake, na yeye atakulaani mbele ya uso Wako.

c. Namna Ayubu Anavyoshughulikia Majaribio

Ayubu 2:9-10 Kisha mkewe akasema kwake, Je, Wewe bado unabaki na ukamilifu wako? mlaani Mungu, ufe. Lakini yeye akasema kwake, Wewe unazungumza mithili ya mmoja wa wanawake walio wapumbavu wanavyozungumza. Ati? tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya? Katika yote haya Ayubu hakutenda dhambi kwa midomo yake.

Ayubu 3:3 Itokomee mbali hiyo siku ambayo nilizaliwa, na huo usiku ambapo ulisemwa, Kuna mtoto mume ameingia katika mimba.

Upendo wa Ayubu wa Njia ya Mungu Unazidi Yote Mengine

Maandiko yanarekodi maneno haya yaliyozungumzwa kati ya Mungu na Shetani: “Naye Yehova akasema kwa Shetani, je, umemfikiria mtumishi Wangu Ayubu, kwamba hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu? Na bado anashikilia ukamilifu wake, ingawa ulinichochea dhidi yake, ili mimi nimwangamize bila sababu” (Ayubu 2:3). Katika maneno haya Mungu Anarudia swali moja kwa Shetani. Ni swali linalotuonyesha ukadiriaji wa uthibitisho wa Yehova Mungu kuhusu kile kilichoonyeshwa na kuishi na kudhihirishwa na Ayubu kwenye jaribio lake la kwanza, na ule ambao si tofauti na ukadiriaji wa Mungu wa Ayubu kabla ya kupitia jaribio lile la Shetani. Hivi ni kusema, kabla jaribio halijamfika, katika macho ya Mungu Ayubu alikuwa mtimilifu, na hivyo basi Mungu Alimlinda yeye na familia yake, na Akambariki, alistahili kubarikiwa kwa macho ya Mungu. Baada ya jaribio, Ayubu hakutenda dhambi kwa midomo yake kwa sababu alikuwa amepoteza mali yake na watoto wake, lakini aliendelea kulisifu jina la Yehova. Mwenendo wake halisi ulimfanya Mungu kumpongeza, na kumpa alama zote. Kwani machoni mwa Ayubu, watoto wake au rasilimali zake hazikutosha kumfanya yeye kumkataa Mungu. Nafasi ya Mungu katika moyo wake, kwa maneno mengine, isingeweza kusawazishwa na watoto wake au kipande chochote cha mali yake. Kwenye jaribio la kwanza la Ayubu, alimwonyesha Mungu kwamba upendo wake kwake na upendo wake wa njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu ulizidi kila kitu kingine. Ni kwa sababu tu jaribio hili lilimpa Ayubu uzoefu wa kupokea tuzo kutoka kwa Yehova Mungu na kufanya mali yake na watoto wake kuchukuliwa na Yeye.

Kwa Ayubu, hali hii aliyoipitia ilikuwa ya kweli na ambayo ilisafisha nafsi yake ikawa safi; ulikuwa ni ubatizo wa maisha uliotimiza uwepo wake, na, isitoshe, ilikuwa ni karamu ya kutosha iliyojaribu utiifu wake kwa, na yeye kumcha Mungu. Jaribio hili lilibadilisha hadhi ya Ayubu kutoka ule wa bwana tajiri hadi kwa mtu ambaye hakuwa na chochote, na pia likamruhusu kupitia dhuluma za shetani kwa wanadamu. Ufukara wake haukumfanya kuchukia Shetani; badala yake, kwenye vitendo vibovu vya Shetani aliuona ubaya na hali ya kudharau ya Shetani pamoja na uadui wa Shetani na uasi wake kwa Mungu, na hali hii ilimhimiza vizuri zaidi kushikilia daima njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Aliapa kwamba asingewahi

kumwacha Mungu na kugeuka njia ya Mungu kwa sababu ya mambo ya nje kama vile mali, watoto au urithi, wala hangewahi kuwa mtumwa wa Shetani, mali, au mtu yeyote; mbali na Yehova Mungu, hakuna mtu ambaye angekuwa Bwana wake, au Mungu wake. Hayo ndiyo yaliyokuwa maazimio ya Ayubu. Kwa upande mwingine wa jaribio, Ayubu alikuwa pia amepata jambo jingine: Alikuwa amepata utajiri mkubwa katikati ya majaribio hayo aliyoyapitia kutoka kwa Mungu.

Wakati wa maisha yake katika miongo kadhaa iliyopita, Ayubu aliyaona matendo ya Yehova na kupata baraka za Yehova Mungu kwake yeye. Zilikuwa ni baraka zilizomwacha akihihi wasiwasi mkubwa na mwenye wingi wa shukrani, kwani aliamini kwamba alikuwa hajamfanyia chochote Mungu, ilhali alikuwa amepata baraka nyingi na akawa anafurahia neema nyingi. Kwa sababu hii, ndani ya moyo wake mara nyingi aliomba, akitumai angeweza kumlipa Mungu, akitumai kwamba angekuwa na fursa ya Kuwa na ushuhuda wa matendo na ukubwa wa Mungu, na kutumai kwamba Mungu angeweza kuujaribu utiifu wake, na, zaidi, kwamba imani yake ingetakaswa, mpaka pale ambapo utiifu wake na imani yake vyote vingepata idhini ya Mungu. Na wakati Ayubu alipojaribiwa, alisadiki kwamba Mungu alikuwa amesikia maombi yake. Ayubu alifurahia sana fursa hii zaidi ya kitu kingine chochote, na hivyo basi hakuthubutu kuchukulia jambo hili vivi hivi, kwani tamanio kubwa zaidi la maisha yake lingetimia. Kufika kwa fursa hii kulimaanisha kwamba utiifu wake na kumcha Mungu vyote vingeweza kutiwa kwenye majaribu, na kutakaswa. Zaidi, ilimaanisha kwamba Ayubu alikuwa na fursa ya kupata idhini ya Mungu, hivyo kumleta karibu zaidi na Mungu. Wakati wa jaribio, imani kama hiyo na kufuatilia huko kulimruhusu yeye kuwa mtimilifu zaidi, na kupata uelewa mkubwa zaidi wa mapenzi ya Mungu. Ayubu alikuwa mwenye shukrani zaidi kwa baraka na neema za Mungu, katika moyo wake alimwaga sifa kubwa zaidi kwa matendo ya Mungu, na alizidi kumcha Mungu na kumstahi, na kutamani hata zaidi upendo, ukubwa, na utakatifu wa Mungu. Wakati huu, ingawaje Ayubu alikuwa bado yuleyule aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu kwenye macho ya Mungu, kuhusiana na yale aliyopitia, imani na maarifa ya Ayubu vyote vilikuwa vimeimarika pakubwa: Imani yake ilikuwa imeongezeka, utiifu wake ulikuwa umeimarika pakubwa, na hali yake ya kumcha Mungu ilikuwa ya kina zaidi. Ingawaje jaribio hili lilibadilisha roho na maisha ya Ayubu, mabadiliko kama hayo hayakumtosheleza Ayubu, wala hayakufanya maendeleo yake ya kwenda mbele kwenda polepole. Wakati huo, akiwa anapiga hesabu kile alichokuwa amepata kutoka kwenye jaribio hilo, na akitilia maanani upungufu wake binafsi, aliomba kimyakimya, akisubiri jaribio linalofuata ambalo lingemsibu yeye, kwa sababu alitamani sana, imani, utiifu, na kumcha Mungu kwake kuweze kuimarishwa kwenye jaribio linalofuata la Mungu.

Mungu Anaziangalia fikira za ndani zaidi za binadamu na yale yote ambayo binadamu

anasema na kufanya. Fikira za Ayubu zilifikia masikio ya Yehova Mungu, na Mungu alisikiliza maombi yake na kwa njia hii jaribio la Mungu kwa Ayubu lililofuata liliwasili kama lilivyotarajiwa.

Katikati ya Mateso makuu, Ayubu Anatambua kwa kweli Utunzaji wa Mungu wa Wanadamu

Kufuatia maswali ya Yehova Mungu kwa Shetani, Shetani alifurahi kisirisiri. Kwa sababu Shetani alijua kwamba angeweza kwa mara nyingine kuruhusiwa kumshambulia mtu aliyekuwa mtimilifu katika macho ya Mungu—jambo ambalo kwa Shetani lilikuwa fursa ya nadra. Shetani alitaka kutumia fursa hii kudhalilisha kabisa kujitolea kwa Ayubu kumfanya kupoteza imani yake kwa Mungu na hivyo basi kutomcha Mungu tena au kubariki jina la Yehova. Hali hii ingempa Shetani fursa: Haijalishi ni wapi au ni muda gani, angeweza kumfanya Ayubu kuwa kikaragosi cha kufuata amri zake. Shetani alificha njama zake za maovu bila kuacha alama, lakini hakuweza kudhibiti asili yake ya maovu. Ukweli huu unaashiriwa kuhusu kupitia kwa majibu yake kwa maneno ya Yehova Mungu, kama yalivyorekodiwa kwenye maandiko. “Naye Shetani akamjibu Yehova, na akasema, Ngozi kwa ngozi, ndiyo, yote ambayo mtu anayo atayatoa kwa sababu ya uhai wake. Lakini nyosha mbele mkono Wako sasa, na uguse mfupa wake na nyama yake, na yeye atakulaani mbele ya uso Wako” (Ayubu 2:4-5). Haiwezekani kutopata maarifa makuu na hali ya kuonea kijicho ya Shetani kutokana na mabadilishano haya kati ya Mungu na Shetani. Baada ya kusikia uongo huu wa Shetani, wale wote wanaoupenda ukweli na kuchukua uovu bila shaka watakuwa na chuki kubwa zaidi kwa utwezo na kutokuwa na aibu kwa Shetani, watahisi wakiwa wametishika na kusinyika kutokana na uongo wa Shetani, na, wakati huohuo, watatoa maombi yao ya kina na heri zao za dhati kwa Ayubu, wakiomba kwamba binadamu huyu mwenye unyofu ataweza kutimiza utimilifu wake, wakitamani kwamba binadamu huyu anayemcha Mungu na kujiepusha na maovu aweze kushinda milele majaribio ya Shetani, na kuishi kwa mwangaza, na kuishi katikati ya mwongozo na baraka za Mungu, hivyo, pia ndivyo watakavyotaka matendo ya haki ya Ayubu yaweze milele kuenea na kuhimiza wale wanaofuatilia njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Ingawaje nia ya kijicho ya Shetani inaweza kuonekana kupitia kwa tangazo hili, Mungu alikubali kwa urahisi “ombi” la Shetani—lakini alikuwa pia na sharti moja: “Yeye yuko katika mkono wako; lakini uuhifadhi uhai wake” (Ayubu 2:6). Kwa sababu, wakati huu, Shetani aliomba kunyosha mbele mkono wake ili kudhuru mwili na mifupa ya Ayubu, Mungu Alisema, “lakini okoa maisha yake.” Maana ya maneno haya ni kwamba alimpa Shetani mwili wa Ayubu, lakini Akabakiza maisha yake. Shetani asingeweza kuyachukua maisha ya Ayubu, lakini isipokuwa haya angeweza kutumia njia au mbinu zozote dhidi ya Ayubu.

Baada ya kupata ruhusa kutoka kwa Mungu, Shetani alimkimbilia Ayubu na kunyosha mbele mkono wake ili kuathiri ngozi yake na akamsababishia majipu mabaya yaliyoupiga mwili wake wote, naye Ayubu akahisi maumivu kwenye ngozi yake. Ayubu aliyasifu maajabu na utakatifu wa Yehova Mungu, jambo ambalo lilimfanya Shetani hata kuwa wazi zaidi katika ufidhuli wake. Kwa sababu alikuwa amehisi furaha ya kumwumiza binadamu, Shetani aliunyoosha mkono wake na akakwaruza nyama ya Ayubu, na kusababisha majipu yake mabaya kutunga usaha. Mara moja Ayubu alihisi maumivu na mateso kwenye mwili wake ambayo hayakuwa na kifani, na asingeweza kujisaidia kwa vyovyote vile isipokuwa kujikanda yeye mwenyewe kutoka kwenye kichwa hadi miguu akitumia mikono yake, ni kana kwamba kufanya hivi kungetuliza balaa ile iliyofanyikia roho yake kutokana na maumivu haya ya nyama za mwili wake. Alitambua kwamba Mungu Alikuwa kando yake akimwangalia, na akajaribu kwa njia bora zaidi kujituliza. Kwa mara nyingine alipiga magoti kwenye ardhi, na kusema: Unaangalia ndani ya binadamu, unauona umaskini wake; kwa nini unyonge wake unakuhusu wewe? Jina la Yehova Mungu lisifiwe. Shetani aliyaona yale maumivu yasiyovumilika ya Ayubu, lakini hakumwona Ayubu akiliacha neno la Yehova Mungu. Hivyo aliunyoosha mkono wake haraka mbele ili kudhuru mifupa ya Ayubu, akiwa na tamaa ya kudhuru kila kiungo cha mwili wake. Mara, Ayubu akahisi mateso asiyoyatarajia; ni kana kwamba mwili wake ulikuwa umepasuliwa katikati kutoka kwenye mifupa, na kana kwamba mifupa yake ilikuwa ikipasuliwa kipande hadi kipande. Mateso haya ya kuumiza yalimfanya akafikiria afadhali basi afe.... uwezo wake wa kuvumilia ulikuwa umefikia kilele.... Alitaka kulia kwa sauti, alitaka kuirarua ngozi kwenye mwili wake ili kupunguza maumivu—lakini alishikilia mayowe yake, na hakuirarua ngozi yake kutoka kwenye mwili wake, kwani hakutaka Shetani auone udhaifu wake. Na hivyo alipiga magoti chini kwa mara nyingine, lakini wakati huu hakuhisi uwepo wa Yehova Mungu. Alijua kwamba mara nyingi alikuwa mbele yake, na nyuma yake, na upande wake. Lakini kwenye maumivu haya, Mungu alikuwa hajawahi kuyatazama; Aliufunika uso wake na Akawa Amefichwa, kwa maana uumbaji wake wa binadamu haukuwa wa kumletea mateso binadamu. Wakati huu, Ayubu alikuwa akilia, na akijaribu kwa njia bora zaidi kuvumilia maumivu yake ya kimwili, lakini asingeweza kujizuia tena dhidi ya kutoa shukrani kwa Mungu: Binadamu aanguka kwa mpigo wa kwanza, yeye ni myonge na asiye na nguvu, yeye ni mchanga na asiyejua—kwa nini ukataka kumtunza na kuwa mzuri kwake yeye? Unanipiga, ilhali inakuumiza kufanya hivyo. Ni nini cha binadamu kinastahili utunzaji na kujali Kwako? Maombi ya Ayubu yalifikia masikio ya Mungu, na ya Mungu Alikuwa kimya, Akitazama tu bila kutoa sauti.... Akiwa amejaribu kila ujanja kwenye kitabu bila mafanikio, Shetani aliondoka kimyakimya, lakini haya hayakufikisha hadi tamati majaribio ya Ayubu kutoka kwa Mungu. Kwa sababu nguvu za Mungu zilizokuwa zimefichuliwa ndani ya Ayubu zilikuwa hazijajulikana kwa umma, hadithi ya Ayubu haikuishia pale ambapo Shetani alijiondoa. Huku wahusika wengine wakiingia

katika tukio hilo, matukio mengine ya ajabu zaidi yalikuwa yaje.

Maonyesho Mengine ya Kumcha Mungu na Kujipusha na Maovu kwa Ayubu ni Kutukuza Kwake Jina la Mungu Katika Mambo Yote

Ayubu alikuwa ameteseka kutokana na maudhi ya Shetani, lakini bado hakuliacha jina la Yehova Mungu. Mke wake ndiye aliyekuwa wa kwanza kujiondoa na kuendeleza wajibu wa Shetani unaoweza kuonekana kwa kumshambulia Ayubu. Maandishi asilia yanafafanua hali hii hivyo basi: “Kisha mkewe akasema kwake, Je, Wewe bado unabaki na ukamilifu wako? mlaani Mungu, ufe” (Ayubu2:9). Haya yalikuwa maneno yaliyozungumzwa na Shetani akisingizia kuwa binadamu. Yalikuwa ni shambulizi, na shtaka, pamoja na kichocheo, jaribio, na matusi. Baada ya kushindwa kushambulia mwili wa Ayubu, Shetani sasa alishambulia moja kwa moja uadilifu wa Ayubu, akitaka kutumia jambo hili kumfanya Ayubu kutupilia mbali uadilifu wake, kumwacha Mungu, na asiendele kuishi tena. Hivyo, pia, ndivyo Shetani alivyotaka kutumia maneno kama hayo kumjaribu Ayubu: Kama Ayubu angeacha jina la Yehova, kisha asingelazimika kuvumilia mateso kama hayo; yeye angejiondolea mateso ya mwili. Akiwa amekabiliwa na ushauri wa mke wake, Ayubu alimkosoa kwa kusema, “Wewe unazungumza mithili ya mmoja wa wanawake walio wapumbavu wanavyozungumza. Ati? tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” (Ayubu 2:10). Ayubu alikuwa amejua kwa muda mrefu maneno haya, lakini wakati huu ukweli wa maarifa ya Ayubu kuhusu maneno haya ulikuwa umethibitishwa.

Wakati mke wake alimshauri kulaani Mungu na kufa, maana yake ilikuwa: “Mungu wako anakushughulikia hivi, kwa hivyo kwa nini usimlaani yeye? Kama ungali hai unafanya nini? Mungu wako hakufanyii haki, na ilhali ungali unasema ‘libarikiwe jina la Yehova’. Angekuletea je janga hili huku unabariki jina Lake? Harakisha na uliache jina la Mungu, na usimfuate yeye tena. Kisha, matatizo yako yataisha.” Kwa wakati huu, ushuhuda ulitolewa ambao Mungu alitaka kuuona kwa Ayubu. Hakuna mtu yeyote wa kawaida ambaye angeweza kuwa na ushuhuda huu, wala hatuusomi katika mojawapo ya hadithi za Biblia—lakini Mungu Alikuwa ameuona kabla hata Ayubu kuongea maneno haya. Mungu Alitaka tu kutumia fursa hii kumruhusu Ayubu kuthibitisha kwa wote kwamba Mungu alikuwa sahihi. Akiwa amekabiliwa na ushauri wa mke wake, Ayubu hakutupilia tu mbali uadilifu wake au kumuacha Mungu, bali pia alimwambia mke wake: “Tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” Je, maneno haya yanao uzito mkuu? Hapa, kunayo ukweli mmoja tu unaoweza kuthibitisha uzito wa maneno haya. Uzito wa maneno haya ni kwamba yameidhinishwa na Mungu ndani ya moyo Wake, ndiyo yale yaliyotamaniwa na Mungu, ndiyo yale Mungu Alitaka kusikia, na ndiyo matokeo ambayo Mungu Alitamani kuona; maneno haya ndiyo pia kiini cha ushuhuda wa Ayubu. Katika haya, utimilifu, unyofu, kumcha Mungu, kujipusha na maovu kwa

Ayubu kulithibitishwa. Thamani ya Ayubu ilikuwa namna ambavyo, alipojaribiwa, na hata wakati mwili wake mzima ulikuwa umefunikwa na majipu mabaya, alipovumilia mateso ya kiwango cha juu zaidi, na wakati mke na watu wake wa ukoo walipomshauri, bado aliyatamka maneno hayo. Ili niweze kuiweka kwa njia nyingine, ndani ya moyo wake alisadiki kwamba, haijalishi ni kiasi kipi cha majaribio, au ni vipi ambavyo masaibu au mateso yalivyokuwa, hata kama kifo kingemjia, hangemuacha Mungu au kugeuka na kuacha kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Unaona, basi, kwamba Mungu Alishikilia sehemu muhimu sana ndani ya moyo wake, na kwamba kulikuwa tu na Mungu moyoni mwake. Ni kwa sababu ya haya ndipo tunasoma ufafanuzi kama huo kuhusu yeye katika maandiko kama: Katika yote haya Ayubu hakutenda dhambi na midomo yake. Hakutenda dhambi kwa kutumia mdomo wake tu, lakini ndani ya moyo wake hakulalamika katu kuhusu Mungu. Hakusema maneno mabaya kuhusu Mungu, wala hakutenda dhambi dhidi ya Mungu. Kinywa chake hakikubariki tu jina la Mungu, lakini ndani ya moyo wake alibariki pia jina la Mungu; mdomo na moyo wake ulikuwa kitu kimoja. Huyu ndiye aliyekuwa Ayubu wa kweli aliyeonekana na Mungu, na hii ndiyo iliyokuwa sababu ya kweli kwa nini Mungu alimthamini sana Ayubu.

Kutoelewa Kwingi Kwa Watu Kuhusu Ayubu

Ugumu aliopitia Ayubu haukuwa kazi ya malaika waliotumwa na Mungu, wala haukusababishwa na mkono wa Mungu mwenyewe. Badala yake, ulisababishwa na Shetani mwenyewe, adui wa Mungu. Hivyo basi, kiwango cha ugumu aliopitia Ayubu kilikuwa kikubwa. Ilhali kwa wakati huo Ayubu alionyesha, kwa moyo mkunjufu, maarifa yake ya kila siku kuhusu Mungu ndani ya moyo wake, kanuni za vitendo vyake vya kila siku, na mwelekeo wake kwa Mungu—na huu ndio ukweli. Kama Ayubu hangekuwa amejaribiwa, kama Mungu Asingekuwa Amemletea Ayubu majaribio, wakati Ayubu aliposema, “Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe,” ungesema kwamba Ayubu alikuwa mnafiki; Mungu alikuwa amempa rasilimali nyingi, hivyo bila shaka alilibariki jina la Yehova. Kama, kabla ya kupitia majaribio, Ayubu angekuwa amesema, “Tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” Ungesema kwamba Ayubu alikuwa akipiga chuku, na kwamba hangeliacha jina la Mungu kwa sababu mara nyingi alibarikiwa kwa mkono wa Mungu. Kama Mungu Angekuwa Amemletea janga, basi kwa kweli angeliacha jina la Mungu. Lakini wakati Ayubu alipojipata katika hali hizi ambazo hakuna yeyote angetaka kujipata ndani au kutaka kuona, au kutaka zimpate, ambazo watu wangeogopa kupata, hali ambazo hata Mungu mwenyewe Hakuweza kuvumilia kuzitazama, bado Ayubu aliweza kushikilia uadilifu wake: “Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe” na “tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” Kama wangekumbwa na mwenendo wa Ayubu wakati huu, wale wanaopenda kuzungumzia maneno ya kuonyesha umuhimu na kuvutia, na wale

wanaopenda kuongea barua na mafundisho ya dini, wote wanaachwa wanyamavu. Wale wanaotukuza jina la Mungu kwa matamshi pekee, ilhali hawajawahi kukubali majaribio ya Mungu, wanashutumiwa na uadilifu ambao Ayubu alishikilia kwa dhati, na wale ambao hawajawahi kusadiki kwamba binadamu anaweza kushikilia kwa dhati njia ya Mungu wanahukumiwa na ushuhuda wa Ayubu. Wakiwa wamekabiliwa na mwenendo wa Ayubu wakati wa majaribio haya na maneno aliyoyaongea, baadhi ya watu watahisi wakiwa wamechanganyikiwa, baadhi watamwonea wivu, baadhi wahisi shaka, baadhi wataonekana hata wasio na haja ya kufuatilia mambo haya, huku wakiukataa ushuhuda wa Ayubu kwa sababu hawayaoni tu mateso yaliyompata Ayubu wakati wa majaribio, na kusoma maneno yaliyozungumzwa na Ayubu, lakini pia ule “unyonge” wa binadamu uliofichuliwa na Ayubu wakati majaribio yalipomsibu. “Unyonge” huu wanaoamini kuwa ile hali ya kudaiwa ya kutokuwa mtimilifu katika utimilifu wa Ayubu, doa katika binadamu ambaye katika macho ya Mungu alikuwa mtimilifu. Hivi ni kusema kwamba, inasadikiwa kwamba wale walio watimilifu hawana doa wala toa, hawana dosari wala hila, kwamba hawana unyonge wowote, hawana habari yoyote kuhusu maumivu, kwamba hawahisi katu wakiwa wamehuzunika au wamekataliwa, na hawana chuki au tabia yoyote ya nje isiyojaa; kutokana na haya, watu wengi hawasadiki kwamba Ayubu alikuwa kwa kweli mtimilifu. Watu hawaidhinishi mambo mengi kuhusu tabia yake wakati wa majaribio yake. Kwa mfano, wakati Ayubu alipopoteza mali yake na watoto wake, hakuweza, kama vile watu wanavyofikiria, kuanza kulia. “Utovu wake wa adabu” unawafanya watu kufikiria alikuwa jiwe, kwani hakuwa na machozi wala upendo kwa familia yake. Hii ndiyo picha mbaya ya kwanza ambayo Ayubu anawaonyesha watu. Wanafikiri tabia yake baada ya hapo kuwa ya kushangaza zaidi: “akalipasua joho lake” ni kauli iliyotafsiriwa na watu kuonyesha utovu wake wa heshima kwa Mungu, na “kunyoa kichwa chake” kunasadikiwa visivyo kumaanisha kukufuru kwa Ayubu na upinzani wake kwa Mungu. Mbali na maneno ya Ayubu kwamba “Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe,” watu hawatambui uhaki wowote ndani ya Ayubu uliosifiwa na Mungu, na hivyo ukadiriaji kuhusu Ayubu uliofanywa na wengi wao si chochote zaidi ya kutofahamu, kutoelewa, shaka, lawama, na idhinisho kwa nadharia tu. Hakuna kati yao anayeweza kuelewa na kushukuru kwa kweli maneno ya Yehova Mungu kwamba Ayubu alikuwa binadamu mtimilifu na mnyofu, yule aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu.

Kutokana na picha yao kuhusu Ayubu hapo juu, watu wana shaka zaidi kuhusiana na uhaki wake, kwani vitendo na mwenendo wa Ayubu uliorekodiwa kwenye maandiko haukuwa wenye mguso wa kina kama vile watu wangefikiria. Hakutekeleza tendo lolote kubwa tu, lakini pia alikichukua kigae ili ajikwaruze akiwa ameketi kwenye jivu. Kitendo hiki kinawashangaza pia watu na kuwafanya kutilia shaka—na hata kukataa—uhaki wa Ayubu, kwani wakati

akijikwaruza Ayubu hakumwomba Mungu, au kutoa ahadi kwa Mungu; wala, zaidi ya hayo, hakuonekana akilia machozi ya maumivu. Wakati huu, watu wanauona tu unyonge wa Ayubu na wala sio chochote kingine, na hivyo hata wanapomsikia Ayubu akisema “Tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” hawaguswi kamwe, au vinginevyo hawaonekani kuamua chochote, na bado hawawezi kutambua uhaki wa Ayubu kutoka kwa maneno haya. Picha ya kimsingi ambayo Ayubu anapatia watu wakati wa mateso ya majaribio yake ni kwamba alikuwa si mnyenyekevu wala mwenye kiburi. Watu hawaioni hadithi inayotokana na tabia yake iliyojitokeza katika kina cha moyo wake, wala hawaioni ile hali yake ya kumcha Mungu ndani ya moyo wake au kutii kwa kanuni ya njia ya kujiepusha na maovu. Utulivu wake unawafanya watu kufikiria kuwa utimilifu na unyofu wake vyote vilikuwa ni maneno matupu tu, kwamba kumcha kwake Mungu kulikuwa tu uvumi; ule “unyonge” alioufichua kwa nje, wakati huo, unawaachia picha ya kina, ukiwapatia “mtazamo mpya” kuhusu, na hata “uelewa mpya” kuhusu binadamu yule ambaye Mungu anafafanua kuwa mtimilifu na mnyofu. “Mtazamo mpya” na “uelewa mpya” kama huo vyote vinathibitishwa wakati Ayubu alipokifungua kichwa chake na kulaani siku aliyojaliwa.

Ingawaje kiwango cha mateso aliyoyapitia hakifikiriki wala kufahamika kwa binadamu yeyote, hakuzungumza maneno yoyote ya uvumi, lakini alipunguza tu maumivu ya mwili wake kwa njia zake mwenyewe. Kama ilivyorekodiwa kwenye maandiko, alisema: “Itokomee mbali hiyo siku ambayo nilizaliwa, na huo usiku ambapo ulisemwa, Kuna mtoto mume ameingia katika mimba” (Ayubu 3:3). Pengine, hakuna yeyote aliyewahi kutilia maanani maneno haya na kuona kwamba ni muhimu, na pengine kuna watu ambao wameyatilia maanani. Kwa maoni yenu, yanamaanisha kwamba Ayubu alimpinga Mungu? Je, ni malalamiko dhidi ya Mungu? Najua kwamba wengi wenu mnayo mawazo fulani kuhusu maneno haya yaliyozungumzwa na Ayubu na mnasadiki kwamba kama Ayubu alikuwa mtimilifu na mnyofu, hakufaa kuonyesha unyonge wowote au huzuni yoyote, na badala yake alifaa kukabiliana vilivyo na shambulizi lolote kutoka kwa Shetani kwa njia nzuri, na hata kutabasamu wakati alikumbwa na majaribio ya Shetani. Hakufaa kuwa na mwikio hata mdogo kuhusiana na mateso aliyoyapata kwenye mwili wake kutokana na Shetani, wala hakufaa kuonyesha hisia zozote ndani ya moyo wake. Alifaa hata kuuliza kwamba Mungu Ayafanye majaribio haya kuwa mabaya zaidi. Haya ndiyo yanayofaa kuonyeshwa na kumilikiwa na mtu ambaye hatikisiki na ambaye anamcha Mungu kwa kweli na kujiepusha na maovu. Katikati ya mateso haya makuu, Ayubu hakufanya chochote ila kulaani siku aliyojaliwa. Hakulalamika kuhusu Mungu, hakuwa na nia yoyote ya kumpinga Mungu. Hali hii ni rahisi zaidi ikisemwa kuliko kutendwa, kwani tangu enzi za zamani hadi wa leo, hakuna yeyote ambaye amewahi kupitia majaribio kama hayo au kuteseka kama vile Ayubu alivyoteseka. Na kwa nini hakuna yeyote ambaye amepitia aina hiyo ya majaribio ya Ayubu?

Kwa sababu, kama vile Mungu Anavyoona, hakuna yeyote anayeweza kuvumilia wajibu au agizo kama hilo, hakuna anayeweza kufanya kama Ayubu alivyofanya, na, zaidi, hakuna yule ambaye bado, mbali na kuilaani siku ya kuzaliwa kwake, anaweza kutoliacha jina la Mungu na kuendelea kubariki jina la Yehova Mungu, kama vile Ayubu alivyofanya wakati mateso kama hayo yalimpata. Je, mtu yeyote angeweza kufanya hivi? Tunaposema haya kumhusu Ayubu, tunapongeza tabia yake? Alikuwa binadamu mwenye haki, na aliyeweza kuwa na ushuhuda kama huo kwa Mungu, aliyeweza kumfanya Shetani kutoroka kwa haraka sana, ili asiwahi kuja mbele ya Mungu tena na kumshtaki yeye—kwa hivyo nini mbaya na kumpongeza? Inaweza kuwa kwamba mnavyo viwango vya juu zaidi kuliko Mungu? Inaweza kuwa kwamba mngechukua hatua hata bora zaidi kuliko Ayubu wakati majaribio yatakapowasibu? Ayubu alisifiwa na Mungu—ni upinzani upi mnaoweza kuwa nao?

Ayubu Anailaani Siku Ya Kuzaliwa Kwake Kwa Sababu Hamtaki Mungu Kupata Maumivu Kwa Sababu Yake

Mara nyingi mimi husema kwamba Mungu huangalia ndani ya mioyo ya watu, na watu huangalia namna watu walivyo kwa nje. Kwa sababu Mungu anaangalia ndani ya mioyo ya watu, Anaelewa kiini chao, huku nao watu wanafafanua kiini cha watu wengine kutokana na wanavyoonekana kwa nje. Wakati Ayubu alipoufunua mdomo wake na kulaani siku ya kuzaliwa kwake, kitendo hiki kilishangaza wahusika wote wa kiroho, wakiwemo wale marafiki watatu wa Ayubu. Binadamu alitoka kwa Mungu, na anafaa kuwa mwenye shukrani kwa maisha na mwili, pamoja na siku yake ya kuzaliwa, aliopewa na Mwenyezi Mungu, na wala hafai kuilaani. Hali hii inaeleweka na kufahamika na watu wengi. Kwa yeyote yule anayemfuata Mungu, uelewa huu ni takatifu na dhabiti, ni ukweli usioweza kubadilika. Ayubu, kwa mkono mwingine, alizivunja sheria: Aliilaani siku ya kuzaliwa kwake. Hiki ni kitendo ambacho watu wa kawaida huchukulia kuwa kinajumuisha kuvuka hadi kwenye eneo haramu. Yeye hastahili tu uelewa na huruma ya watu, lakini pia hastahili msamaha wa Mungu. Wakati huohuo, hata watu wengi zaidi wanatilia shaka uhaki wa Ayubu, kwani inaonekana kana kwamba kibali cha Mungu kwake yeye kilimfanya Ayubu kujifikiria yeye mwenyewe, kilimfanya kuwa jasiri sana na asiyejali kiasi cha kwamba hakuweza tu kutoshukuru Mungu kwa kumbariki yeye na kumtunza yeye wakati wa maisha yake, lakini pia aliilaani siku ya kuzaliwa kwake na kuomba ingeangamizwa. Hii ni nini, kama si kumpinga Mungu? Mambo ya juujuu kama hayo yanawapa watu ithibati ya kushutumu kitendo hiki cha Ayubu, lakini ni nani anayejua kile Ayubu alichokuwa akifikiria kwa kweli wakati huo? Na ni nani anayeweza kujua sababu ya Ayubu kufanya hivyo? Mungu pekee na Ayubu mwenyewe ndio wanaojua hadithi ya ndani na sababu husika hapa.

Wakati Shetani alipounyosha mbele mkono wake ili kudhuru mifupa ya Ayubu, Ayubu

aliangukia mashiko yake, bila ya mbinu za kutoroka au nguvu za kumpinga. Mwili na nafsi yake iliteseka na kupata maumivu makali, na maumivu haya yalimfanya kufahamu kwa kina kuhusu kutokuwa na umuhimu, unyonge, na hali ya kutokuwa na mamlaka iliyokuwemo ndani ya mwili. Wakati huohuo, alipata shukrani na uelewa mkubwa wa kwa nini Mungu Anatilia maanani kujali na kutunza wanadamu. Akiwa ameangukia mashiko ya Shetani, Ayubu alitambua kwamba binadamu, aliye katika mwili na damu, kwa hakika hana nguvu kamwe. Wakati aliposujudu na kumwomba Mungu, alihisi ni kana kwamba Mungu Alikuwa akiufunika uso Wake na kujificha, kwani Mungu Alikuwa Amemweka kabisa katika mikono ya Shetani. Wakati huohuo, Mungu Alimlilia yeye, na, zaidi, Alimsikitikia yeye; Mungu Aliumizwa na maumivu yake na Aliumia kwa maumivu yake.... Ayubu alihisi maumivu ya Mungu, pamoja na namna ambavyo haikuweza kuvumilika kwa Mungu.... Ayubu hakutaka kuleta huzuni wowote zaidi kwa Mungu, wala hakutaka Mungu kulia kwa ajili yake yeye, isitoshe hakutaka kumwona Mungu akiwa katika maumivu kwa sababu yake yeye. Wakati huu, Ayubu alitaka tu kujiondoa mwenyewe kwenye mwili wake, kuacha kuvumilia tena maumivu yaliyoletewa kwake kupitia kwa mwili wake, kwani kufanya hivi kungekomesha Mungu kuteseka kwa maumivu yake—lakini hakuweza kufanya hivyo, na alifaa kuvumilia tu maumivu ya mwili, na pia mateso ya kutotaka kumfanya Mungu kuwa na wasiwasi. Maumivu haya mawili—moja kutoka kwa mwili, na mengine kutoka kwa roho—yalileta maumivu makali ya moyoni, yakusokotesha tumbo kwake Ayubu, na kumfanya yeye kuhisi namna ambavyo mipaka ya binadamu aliye na mwili na damu inavyoweza kumfanya mtu kuhisi akiwa amedhalilishwa na asiye na njia ya kusaidika. Katika hali hizi, tamanio lake la Mungu lilizidi kukua, na chuki yake kwa Shetani ikazidi kuwa nyingi. Wakati huu, Ayubu angependelea kutowahi kuzaliwa kwenye ulimwengu huu wa binadamu, afadhali asingekuwepo badala ya kumuona Mungu Akilia au Akihisi maumivu kwa sababu yake. Alianza kuchukia kwa kina mwili wake, kuwa mgonjwa na mchovu ndani yake mwenyewe, siku yake ya kuzaliwa, na hata ya hayo yote ambayo yalikuwa yameunganishwa kwake. Hakutaka kuwepo na kutajwa kokote zaidi kuhusu siku yake ya kuzaliwa au chochote kilichohusu siku hiyo, na hivyo aliufunua mdomo wake na kuilaani siku yake ya kuzaliwa: “Itokomee mbali hiyo siku ambayo nilizaliwa, na huo usiku ambapo ulisemwa, Kuna mtoto mume ameingia katika mimba. Siku ile iwe na kiza; Mungu na asiitazame kutoka juu, wala nuru iiangazie” (Ayubu 3:3-4). Maneno ya Ayubu yanaonyesha kuchukia kwake kwa nafsi yake mwenyewe, “Itokomee mbali hiyo siku ambayo nilizaliwa, na huo usiku ambapo ulisemwa, Kuna mtoto mume ameingia katika mimba,” pamoja na yeye kujilaumu mwenyewe na kuwa katika hali ya kuhisi kwamba yuko katika hatia kwa kumsababishia Mungu maumivu, “Siku ile iwe na kiza; Mungu na asiitazame kutoka juu, wala nuru iiangazie.” Vifungu hivi viwili ni maonyesho ya namna Ayubu alivyohisi wakati huo, na vinaonyesha kikamilifu utimilifu wake na unyofu wake kwa wote. Wakati huohuo, kama vile tu Ayubu alivyokuwa ametaka, imani na utiifu wake kwa Mungu,

pamoja na kumcha Mungu kwake, vyote viliinuliwa. Bila shaka, kuinuliwa huku kwa hakika ni athari ambayo Mungu Alikuwa Ametarajia.

Ayubu Amshinda Shetani na Kuwa Binadamu Wa Kweli Machoni pa Mungu

Wakati Ayubu alipopitia majaribio yake kwa mara ya kwanza, alinyang'anywa mali yake yote na watoto wake wote, lakini hakujisujudia na kusema chochote ambacho kilikuwa dhambi dhidi ya Mungu kutokana na hayo. Alikuwa ameshinda majaribio ya Shetani, na alikuwa ameshinda rasilimali zake zote za dunia na watoto wake, na majaribio ya kupoteza mali yake ya dunia, hivi ni kusema kwamba aliweza kutii Mungu kuchukua na kutwaa kutoka kwake na akatoa shukrani na sifa kwa Mungu kwa sababu ya hayo. Hivyo ndivyo ulivyokuwa mwenendo wa Ayubu wakati wa jaribio la kwanza la Shetani, na huo ndio uliokuwa ushuhuda wa Ayubu wakati wa jaribio la kwanza la Mungu. Kwenye jaribio la pili, Shetani aliunyosha mbele mkono wake ili kumdhuru Ayubu, na ingawaje Ayubu alipitia maumivu yaliyokuwa makubwa zaidi kuliko yale aliyokuwa amepitia awali, bado ushuhuda wake ulikuwa wa kutosha wa kuacha watu wakiwa wameshangazwa. Alitumia ujasiri wake, imani yake, na utiifu kwa Mungu, pamoja na kumcha Mungu kwake, kwa mara nyingine tena kumshinda Shetani, na mwenendo wake na ushuhuda wake viliweza kwa mara nyingine tena kuidhinishwa na kupata kibali cha Mungu. Wakati wa majaribio haya, Ayubu alitumia mwenendo wake halisi kumtangazia Shetani kwamba maumivu ya mwili wake yasingebadilisha imani yake na utiifu wake kwa Mungu au kuchukua ule upendo wake kwa Mungu na kumcha Mungu; asingemuacha Mungu au kutupilia mbali utimilifu wake binafsi na unyofu kwa sababu alikuwa amekabiliwa na kifo. Bidii ya Ayubu ilimfanya Shetani mwoga, imani yake ilimuacha Shetani akiwa na dukuduku na kutetemeka, nguvu za vita vya maisha yake na kifo chake na Shetani viliweza kuzua chuki na dharau nyingi kwa Shetani, utimilifu na unyofu wake ulimuacha Shetani akiwa hana chochote zaidi cha kumfanya kiasi cha kwamba Shetani aliyaacha mashambulizi yake kwake na kukata tamaa na mashtaka yake dhidi ya Ayubu mbele ya Yehova Mungu. Hii ilimaanisha kwamba Ayubu alikuwa ameushinda ulimwengu, alikuwa ameushinda mwili wake, alikuwa amemshinda Shetani, na alikuwa ameshinda kifo; alikuwa kwa kweli na hakika binadamu aliyemilikiwa na Mungu. Wakati wa majaribio haya mawili, Ayubu alisimama imara katika ushuhuda wake, na kwa hakika aliishi kwa kudhihirisha utimilifu wake na unyofu, na akapanua upana wa kanuni zake za kuishi za kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Baada ya kupitia majaribio haya mawili, ndani ya Ayubu kulizaliwa uzoefu mwingi, na uzoefu huu ulimfanya yeye kuwa mwenye kimo na uzoefu zaidi, ilimfanya kuwa mwenye nguvu zaidi, na imani kubwa zaidi, na ilimfanya yeye kuwa na ujasiri zaidi kuhusu haki na ustahili wa uadilifu ambao yeye alishikilia kwa dhati. Majaribio ya Yehova Mungu kwa Ayubu yalimpa uelewa wa kina na hisia za wasiwasi wa Mungu kwa binadamu, na kumruhusu yeye kuhisi thamani ya upendo wa Mungu,

ambapo vyote vinaelekezwa katika utiliaji maanani kwa na kuhusu upendo wa Mungu na vyote viliweza kuongezwa katika kumcha Mungu. Majaribio ya Yehova Mungu kumwondoa tu Ayubu kutoka Kwake, lakini pia yaliuleta moyo wake karibu na Mungu. Wakati maumivu yale ya mwili yaliyovumiliwa na Ayubu yalifikia kilele, wasiwasi aliouhisi kutoka kwa Yehova Mungu haukumpa chaguo lolote ila kuilaani siku yake ya kuzaliwa. Mwenendo kama huo haukuwa umepangiliwa mapema lakini ulikuwa ni ufunuo wa kiasili wa kutilia maanani na kumpenda Mungu kutoka ndani ya moyo wake, ulikuwa ni ufunuo wa kiasili uliotoka kwenye kutilia maanani na kumpenda Mungu kwake. Hivi ni kusema, kwa sababu alijichukia, na hakuwa na radhi na hakuweza kuvumilia kuona Mungu Akiteswa, hivyo kutilia maanani na upendo wake vilifika hali ya kutojijali. Wakati huu, Ayubu aliimarisha kuabudu kwake kwa muda mrefu na kutamani kwake kwa Mungu na upendo kwa Mungu hadi katika kiwango cha utiliaji maanani na upendo. Wakati huohuo, aliweza kupandisha imani na utiifu wake kwa Mungu na kumcha Mungu kwake hadi katika kiwango cha kutilia maanani na upendo. Hakujiruhusu kufanya chochote ambacho kingesababisha madhara kwa Mungu, hakujiruhusu mwenendo ambao ungemuumiza Mungu, na hakujiruhusu kuleta masikitiko, huzuni au hata kutokuwa na furaha kokote kwake Mungu kwa sababu zake mwenyewe. Katika Macho ya Mungu, ingawaje Ayubu alikuwa bado Ayubu wa hapo awali, imani, utiifu na kumcha Mungu kwake kulikuwa kumemletea Mungu utoshelezi kamilifu. Wakati huu, Mungu alitarajia Ayubu kuweza kutimiza, alikuwa amegeuka kuwa mtu aliyestahili kuitwa “mtimilifu na mnyofu” mbele ya macho ya Mungu. Vitendo vyake vya haki vilimruhusu yeye kumshinda Shetani na kuwa makini katika ushuhuda wake kwa Mungu. Hivyo, pia, matendo yake ya haki yalimfanya kuwa mtimilifu, na kuruhusu thamani ya maisha yake kuimarishwa, kuzidishwa zaidi kuliko awali, na kumfanya yeye kuwa mtu wa kwanza kutoweza kushambuliwa au kujaribiwa zaidi na Shetani. Kwa sababu Ayubu alikuwa mwenye haki, alishtakiwa na kujaribiwa na Shetani; kwa sababu Ayubu alikuwa mwenye haki, alikabidhiwa Shetani; na kwa sababu Ayubu alikuwa mwenye haki, alishinda na kumlelea Shetani, na kuweza kusimama imara katika ushuhuda wake. Kuendelea mbele, Ayubu akawa binadamu wa kwanza ambaye hangewahi tena kukabidhiwa Shetani, kwa kweli alikuja mbele ya kiti cha enzi cha Mungu na akaishi kwenye nuru, katika baraka za Mungu bila ya kupelelezwa au kuangamizwa na Shetani.... Alikuwa amekuwa binadamu wa kweli katika macho ya Mungu; alikuwa ameachiliwa huru. ...

Kuhusu Ayubu

Baada ya kusikia namna Ayubu alivyopitia majaribio, kunao uwezekano kwamba wengi wenu watataka kujua maelezo zaidi kuhusu Ayubu mwenyewe, hasa kuhusiana na siri iliyomfanya akapata sifa za Mungu. Hivyo basi leo, hebu tuzungumzie kuhusu Ayubu!

Katika Maisha ya Kila Siku ya Ayubu Tunaona Utimilifu, Unyofu, Kumcha Mungu, na Kujiepusha na Maovu Kwake

Kama tutazungumzia Ayubu, basi lazima tuanze na namna ambavyo alitathminiwa kwa mujibu wa matamshi kutoka kwa kinywa cha Mungu mwenyewe: “Hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu.”

Hebu kwanza tujifunze kuhusu utimilifu na unyofu wa Ayubu.

Unaelewa vipi maneno haya “utimilifu” na “unyofu”? Unasadiki kwamba Ayubu hakuwa na lawama, na kwamba aliheshimika? Hili, bila shaka, litakuwa ni ufasiri wa moja kwa moja na uelewa wa “mtimilifu” na “mnyofu.” Muhimu katika uelewa wa kweli wa Ayubu ni maisha halisi—maneno, vitabu, na nadharia pekee haviwezi kutupa majibu yoyote. Tutaanza na kuyaangalia maisha ya Ayubu ya nyumbani, kuangalia namna mwenendo wake wa kawaida ulivyokuwa maishani mwake. Kufanya hivi kutatwambia kuhusu kanuni na malengo yake maishani, pamoja na hulka yake na mambo yale aliyoyafuatilia. Sasa, hebu tuyasome maneno ya mwisho katika Ayubu 1:3: “Mtu huyo alikuwa mkubwa zaidi kuwaliko watu wengine wote wa mashariki.” Kile ambacho maneno haya yanasema ni kwamba hadhi na heshima ya Ayubu ilikuwa ya juu sana, na ingawaje hatuambiwi kama alikuwa ndiye mkubwa zaidi kati ya wanaume wote wa mashariki kwa sababu ya wingi wa rasilimali zake au kwa sababu alikuwa mtimilifu na mnyofu, na kwamba alimcha Mungu na kujiepusha na maovu, kwa ujumla tunajua kwamba hadhi na heshima ya Ayubu vyote vilithaminiwa sana. Kama ilivyorekodiwa kwenye Biblia, picha za kwanza za Ayubu kwa watu zilikuwa kwamba Ayubu alikuwa mtimilifu, kwamba alimcha Mungu na kujiepusha na maovu na kwamba alimiliki utajiri mkubwa na alikuwa na hadhi ya kuheshimika. Kwa mtu wa kawaida anayeishi katika mazingira kama haya na hali kama hizo, mlo wa Ayubu, ubora wa maisha, na vipengele mbalimbali vya maisha yake ya kibinafsi vyote vingekuwa malengo ya umakinifu wa watu wengi; hivyo lazima tuendeleo kuyasoma maandiko: “Nao wana wake walienda na kufurahia karamu katika nyumba zao, kila kwa siku yake; na wao wakatuma na kuwaita ndugu zao wa kike watatu ili wakule na kunywa pamoja na wao. Na ilikuwa hivyo, wakati hizo siku zao za karamu ziliisha, Ayubu aliwatuma na kuwatakasa, na akaamka asubuhi mapema, na kutoa sadaka za kuteketezwa kulingana na hesabu yao wote; kwa sababu Ayubu alisema, Inaweza kuwa kwamba wana wangu wametenda dhambi, na kumlaani Mungu mioyoni mwao. Hivyo ndivyo Ayubu alivyofanya kila siku” (Ayubu 1:4-5). Kifungu hiki kinatuambia mambo mawili: Jambo la kwanza ni kwamba watoto wa kiume na wa kike wa Ayubu walishiriki kwenye karamu mara kwa mara, wakila na wakinywa; pili ni kwamba Ayubu mara kwa mara alitoa sadaka za kuteketezwa kwa sababu alikuwa na wasiwasi na wao, akiogopa kwamba walikuwa wakitenda dhambi, kwamba katika mioyo yao walikuwa

wamemlaani Mungu. Katika maandiko haya maisha ya watu wa aina mbili tofauti yanafafanuliwa. Maisha ya kwanza, watoto wa kiume na kike wa Ayubu, mara nyingi walishiriki kwenye karamu kwa sababu ya ukwasi wao, waliishi kwa ubadhirifu, wakinywa na wakila hadi mioyo yao kutosheka, wakifurahia maisha ya kiwango cha juu yaliyoletwa na utajiri wa anasa. Wakiishi maisha kama haya, ilikuwa lazima kwamba mara kwa mara wangetenda dhambi na kumkosea Mungu—ilihali hawakujitakasa wala kutoa sadaka za kuteketezwa kutokana na hayo yote. Waona, basi, kwamba Mungu hakuwa na nafasi katika mioyo yao, kwamba hawakufikiria kuhusu neema za Mungu, wala kuogopa kumkosea Mungu, isitoshe hawakuogopa kumuacha Mungu katika mioyo yao. Bila shaka zingatia letu si watoto wa Ayubu, lakini ni kwa kile ambacho Ayubu alifanya alipokabiliwa na mambo kama haya; hili ndilo suala lile jingine lililofafanuliwa katika kifungu, na ambalo linahusisha maisha ya kila siku ya Ayubu na kiini cha ubinadamu wake. Wakati Biblia inapofafanua kushiriki kwa watoto wa kike na kiume katika karamu mbalimbali hakuna mahali ambapo Ayubu anatajwa; yasemekana tu kuwa ni watoto wake wa kiume na wa kike walio kula na kunywa pamoja. Kwa maneno mengine, hakuandaa karamu, wala hakujiunga na watoto wake wa kiume na kike katika karamu hizo ili kuendeleza ubadhirifu. Ingawaje alikuwa tajiri na alimiliki raslimali nyingi na watumishi wengi, maisha ya Ayubu hayakuwa ya anasa. Hakudanganywa na mazingira yake ya juu kabisa aliyoyaishi na wala hakujiwa na ulafi wa anasa za mwili au kusahau kutoa sadaka za kuteketezwa kwa sababu za utajiri wake, isitoshe pia haya yote hayakumsababisha kuanza kujiepusha na Mungu ndani ya moyo wake kwa utaratibu. Ni dhahiri, hivyo basi, kwamba Ayubu alikuwa na nidhamu katika hali ya maisha yake, wala hakuwa mlafi au na imani ya kuwa anasa kutokana na baraka za Mungu kwake, na hakushikilia na kupumbazwa na ubora wa maisha. Badala yake, alinyenyekea na akawa asiye na majivuno, hakuwa mwenye kujidai na alikuwa mtulivu na makini mbele ya Mungu. Mara nyingi alifikiria kuhusu neema na baraka za Mungu, na siku zote alimcha Mungu. Katika maisha yake ya kila siku, Ayubu mara nyingi alirauka mapema ili kutoa sadaka zilizoteketezwa kwa niaba ya watoto wake wa kiume na kike. Kwa maneno mengine, Ayubu mwenyewe alimcha Mungu na pia alitumaini kwamba watoto wake wangeweza vilevile kumcha Mungu na kutotenda dhambi dhidi ya Mungu. Utajiri wa anasa wa Ayubu haukuwa na mahali popote ndani ya moyo wake, wala haukusawazisha ile nafasi iliyoshikiliwa na Mungu; haijalishi kama ilikuwa ni kwa ajili yake mwenyewe au watoto wake, vitendo vyote vya kila siku vya Ayubu viliunganishwa katika kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Kumcha Yehova Mungu kwake hakukuishia kwenye kinywa chake lakini kulitiwa katika vitendo, na kukajionyesha katika kila sehemu ya maisha yake. Mwenendo huu halisi wa Ayubu unatuonyesha kwamba alikuwa mwaminifu, na alimiliki kiini kilichopenda haki na mambo yaliyokuwa mazuri. Kwamba Ayubu mara nyingi alituma sadaka ya kuwateketeza na kwa niaba ya watoto wake wa kiume na kike na kuwatakaswa kunamaanisha kwamba hakuruhusu wala kuidhinisha tabia ya watoto wake; badala

yake katika moyo wake alichoshwa na tabia yao, na akawashutumu vikali. Alikuwa amethibitisha kwamba tabia ya watoto wake wa kike na kiume haikupendeza Yehova Mungu na hivyo basi mara nyingi aliwaita kwenda mbele ya Yehova Mungu na kutubu dhambi zao. Vitendo vya Ayubu vinatuonyesha upande mwingine wa ubinadamu wake: ule ambao unaonyesha kwamba hakuwahi kutembea na wale ambao mara nyingi walitenda dhambi na kumkosea Mungu, lakini badala yake alijiepusha na kutotaka kuwa nao. Hata ingawaje watu hawa walikuwa watoto wake wa kike na kiume, hakuziacha kanuni zake za kibinafsi kwa sababu walikuwa ukoo wake binafsi wala hakujihusisha kwa dhambi zao kwa sababu ya hisia zake binafsi za moyoni. Badala yake aliwasihi kutubu na kupata ustahimilivu wa Yehova Mungu na akawaonya kutomwacha Mungu kwa ajili ya kujifurahisha kwao kwa ulafi. Kanuni za namna ambavyo Ayubu aliwashughulikia wengine haziwezi kutenganishwa na zile kanuni za kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Alipenda kile kilichokubalika na Mungu na kuchukia kile Alichokiona Mungu kuwa mbaya, na akawapenda wale waliomcha Mungu katika mioyo yao, na kuchukia wale waliotenda maovu au kutenda dhambi dhidi ya Mungu. Upendo na chuki kama hiyo zilionyeshwa katika maisha yake ya kila siku, na ndio uliokuwa unyofu wenyewe wa Ayubu ulioonekana katika macho ya Mungu. Kiasili, haya pia ndiyo maonyesho na kuishi kulingana na ubinadamu wa kweli wa Ayubu katika mahusiano yake na wengine katika maisha yake ya kila siku ambao lazima tujifunze kuhusu.

Maonyesho ya Ubinadamu wa Ayubu Wakati wa Majaribio Yake (Kuelewa Utimilifu wa Ayubu, Unyofu, Kumcha Mungu na Kujiepusha na Maovu Wakati wa Majaribio Yake)

Kile tulichozungumzia hapo juu ni vipengele mbalimbali vya ubinadamu wa Ayubu zilizoonyeshwa katika maisha yake ya kila siku kabla ya majaribio yake. Bila shaka, maonyesho haya mbalimbali yanatupa ufahamu wa mwanzo pamoja na uelewa wa unyofu wa Ayubu, kumcha Mungu na kujiepusha na maovu kwake, na unatupa uthibitisho wa mwanzo. Sababu inayonifanya kusema “mwanzo” ni kwa kuwa watu wengi bado hawana uelewa wa kweli wa hulka ya Ayubu na kiwango ambacho alifuatilia njia ya kutii na kumcha Mungu. Hivi ni kusema, ufahamu wa watu wengi kuhusu Ayubu hauendi kwa kina zaidi ya ile picha ambayo kwa kiasi fulani inamfaa yeye kama ilivyoielezwa katika vifungu viwili kwenye Biblia vilivyo na maneno yake “Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe” na “tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” Hivyo, kunayo haja kubwa yetu sisi kuelewa namna ambavyo Ayubu aliishi kwa kudhihirisha ubinadamu wake alipokuwa akipokea majaribu ya Mungu; kwa njia hii, ubinadamu wote wa kweli wa Ayubu utaweza kuonyeshwa kwa wote.

Wakati Ayubu aliposikia kwamba mali yake ilikuwa imeibwa, kwamba watoto wake wa

kike na kiume walikuwa wameaga dunia, na kwamba watumishi wake walikuwa wameuliwa, aliitikia hivi: “Kutoka hapo Ayubu akainuka, na akalipasua joho lake, na akanyoa kichwa chake, na akaanguka chini, na kuabudu” (Ayubu 1:20). Maneno haya yanatuambia ukweli mmoja: Baada ya kuzisikiza habari hizi, Ayubu hakushikwa na wasiwasi, hakulia au kuwalaumu wale watumishi ambao walikuwa wamempa habari hizo, isitoshe hakukagua eneo la uhalifu ili kuchunguza na kuthibitisha ni kwa nini na ni vipi hali ilikuwa hivyo na kutaka kujua ni nini haswa kilichofanyika. Hakuonyesha maumivu au majuto yoyote kutokana na kupoteza mali yake wala hakuanza kupukutikwa na machozi kutokana na kuwapoteza watoto wake, wapendwa wake. Kinyume ni kwamba, akalirarua joho lake kisha akanyoa kichwa chake, na kuanguka chini, na kuabudu. Vitendo vya Ayubu ni tofauti sana na vile vya binadamu wa kawaida. Vinawachanganya watu wengi, na kuwaruhusu kumkosoa Ayubu ndani ya mioyo yao kwa “kukosa huruma na rehema”. Kwa kupotea ghafla kwa mali yao, watu wa kawaida wangeonekana wamevunjwa moyo, au wanasikitika kweli—au kama ilivyo kwa baadhi ya watu, wanaweza hata kujipata wakiwa wamefadhaishwa moyo. Hii ni kwa sababu, katika mioyo yao, mali ya watu inawakilisha jitihada ya maisha yao yote—ndiyo ambayo maisha yao yanategemea, ndilo tumaini linalowafanya kuishi; kupoteza mali yao kunamaanisha jitihada zao zimeambulia patupu na kwamba hawana tumaini tena na kwamba pia hawana siku za usoni. Huu ndio mwelekeo wa mtu yeyote wa kawaida kuhusiana na mali yake na uhusiano wa karibu alio na mali hiyo, na huu ndio pia umuhimu wa mali katika macho ya watu. Hivyo, idadi kubwa ya watu wanahisi wakiwa wamechanganyikiwa na mtazamo mtulivu wa Ayubu kuhusiana na kupoteza mali yake. Leo, tutauondoa mkanganyiko ambao watu wote walihisi kwa kuelezea kile kilichokuwa kikipitia moyoni mwa Ayubu.

Akili za kawaida zinakariri kwamba, kwa kuwa alikuwa amepewa rasilimali hizo nyingi na Mungu, Ayubu anafaa kuaibika mbele ya Mungu kwa sababu ya kuzipoteza rasilimali hizi, kwani alikuwa hajazitunza, alikuwa hajashikilia zile rasilimali alizopewa na Mungu. Hivyo, aliposikia kwamba mali yake ilikuwa imeibwa, mwitikio wake wa kwanza ulifaa kuwa kuenda kwenye eneo la uhalifu na kuchukua hesabu ya kila kitu kilichokuwa kimepotea na kisha kutubu kwa Mungu ili aweze kwa mara nyingine kupokea baraka za Mungu. Ayubu, hata hivyo hakufanya hivi, na kiasili alikuwa na sababu zake za kutofanya hivyo. Ndani ya Moyo wake, Ayubu alisadiki pakubwa kwamba kila kitu alichomiliki alikuwa amepewa na Mungu na hakikuwa kimetokana na jitihada zake yeye mwenyewe. Hivyo, hakuziona baraka hizo kama jambo la kutilia maanani, lakini alishikilia ile njia alifaa kuchukua kwa udi na uvumba kama kanuni zake za kuishi. Alizitunza baraka za Mungu, na akatoa shukrani kutokana nazo, lakini hakutamanishwa nazo wala hakutafuta baraka zaidi. Huo ndio uliokuwa mwelekeo wake kuhusu mali. Hakufanya chochote kwa minajili ya kupata baraka, wala kuwa na wasiwasi kuhusu au

kuhuzunishwa kutokana na ukosefu au kupoteza baraka za Mungu; hakufurahi kwa njia ya kupindukia na isiyo na mipaka kwa sababu ya baraka za Mungu na wala hakupuuza njia ya Mungu wala kusahau neema ya Mungu kwa sababu ya zile baraka ambazo alifurahia mara kwa mara. Mtazamo wa Ayubu kwa mali yake unafichulia watu ubinadamu wake wa kweli: Kwanza, Ayubu hakuwa binadamu mlaifi, na hakuwa na madai katika maisha yake yakinifu. Pili, Ayubu hakuwahi kuwa na wasiwasi au kuogopa kwamba Mungu angechukua kila kitu alichokuwa nacho, na ndio uliokuwa mwelekeo wake wa utiifu kwa Mungu ndani ya moyo wake; yaani, hakuwa na madai au malalamiko kuhusu ni lini au kama Mungu angechukua kutoka kwake, na wala hakuuliza sababu, lakini alilenga tu kutii mipango ya Mungu. Tatu, hakuwahi kusadiki kwamba rasilimali zake zilitokana na jitihada zake, lakini kwamba alipewa yeye na Mungu. Hii ilikuwa imani ya Ayubu kwa Mungu, na onyesho la imani yake. Je, ubinadamu wa Ayubu na ufuatiliaji wake wa kweli wa kila siku umefanywa kuwa wazi katika muhtasari huu wa hoja tatu kumhusu yeye? Ubinadamu na ufuatiliaji wa Ayubu ni vitu vilivyokuwa muhimu katika mwenendo wake mtulivu alipokabiliwa na hali ya kupoteza mali yake. Ilikuwa hasa kwa sababu ya ufuatiliaji wake wa kila siku ndipo Ayubu akawa na kimo na imani ya kusema, “Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe,” kwenye majaribio ya Mungu. Maneno haya hayakupatwa kwa mkisha mmoja, na wala hayakujitokeza tu kwa ghafla kwenye kichwa chake Ayubu. Yalikuwa yale ambayo alikuwa ameona na kupata kwa miaka mingi ya kupitia safari ya maisha. Akilinganishwa na wale wote wanaotafuta tu baraka za Mungu na wanaogopa Mungu atachukua kutoka kwao, nao wanachukia hali hio na wanalalamikia kuhusu hali hiyo, je utiifu wa Ayubu ni wa kweli haswa? Tukilinganisha na wale wote wanaosadiki kwamba Mungu yupo, lakini ambao hawajawahi kusadiki kwamba Mungu anatawala mambo yote, Ayubu anamiliki uaminifu na unyofu mkubwa?

Urazini wa Ayubu

Uzoefu halisi wa Ayubu na ubinadamu wake wenye unyofu na uaminifu ulimaanisha kwamba alifanya uamuzi na uchaguzi wenye urazini zaidi alipozipoteza rasilimali zake na watoto wake. Machaguo kama hayo ya kirazini yasingeweza kutenganishwa na shughuli zake za kila siku na vitendo vya Mungu ambavyo alikuwa amejua kwenye maisha yake ya siku baada ya siku. Uaminifu wa Ayubu ulimfanya kuweza kusadiki kwamba mkono wa Yehova unatawala mambo yote; imani yake ilimruhusu kujua ukweli wa ukuu wa Yehova Mungu juu ya vitu vyote; maarifa yake yalimfanya kuwa radhi na kuwa na uwezo wa kutii ukuu na mipangilio ya Yehova Mungu juu ya vitu vyote; utiifu wake ulimwezesha kuwa mkweli na mkweli zaidi katika kumcha kwake kwa Yehova Mungu; kumcha kwake kulimfanya kuwa halisi zaidi na zaidi katika kujiepusha kwake na maovu; hatimaye, Ayubu alikuwa mtimilifu kwa sababu alimcha Mungu na kujiepusha na maovu; na ukamilifu kwake kulimfanya kuwa na hekima zaidi na kukampa urazini

wa kipekee.

Tunafaa kulielewa vipi neno hili, “urazini”? Ufasiri wa moja kwa moja unamaanisha kwamba kuwa mwenye hisia nzuri, kuwa mwenye mantiki na wa kueleweka katika kufikiria kwako, kuwa na maneno ya kueleweka, vitendo na hukumu ya kueleweka, na kumiliki viwango visivyo na makosa na maadili ya mara kwa mara. Lakini urazini wa Ayubu hauielezwi sana kwa urahisi. Inaposemekana hapa kwamba Ayubu alimiliki urazini wa kipekee, inahusiana na ubinadamu wake na mwenendo wake mbele ya Mungu. Kwa sababu Ayubu alikuwa mwaminifu, aliweza kuusadiki na kuutii ukuu wa Mungu, uliomba maarifa ambayo yasingeweza kupatikana na wengine na maarifa haya yalimfanya kuweza kutambua, kuhukumu, na kufafanua kwa usahihi zaidi yale yaliyompata, na yaliyomwezesha kuchagua ni nini cha kufanya na ni nini cha kushikilia kwa usahihi na wepesi zaidi wa kukata ushauri. Hivi ni kusema kwamba maneno, tabia, na kanuni zake ziliandamana na hatua zake, na msimbo ambao aliufanyia kazi, ulikuwa wa mara kwa mara, ulio wazi, na mahususi na haukukosa mwelekeo, wenye uamuzi wa haraka au wa kihisia. Alijua namna ya kushughulikia chochote kile kilichompata yeye, alijua namna ya kusawazisha na kushughulikia mahusiano kati ya matukio magumu, alijua namna ya kushikilia mambo kwa njia ambayo mambo hayo yalifaa kushikiliwa, na, vilevile, alijua namna ya kushughulikia ule utoaji na uchukuaji wa Yehova Mungu. Huu ndio uliokuwa urazini wenyewe wa Ayubu. Ilikuwa hasa kwa sababu Ayubu alijihami na urazini kama huu ndiposa akasema, “Yehova alinipa, na Yehova amechukua; jina la Yehova libarikiwe,” alipozipoteza rasilimali zake na watoto wake wa kiume na kike.

Wakati Ayubu alipokabiliwa na maumivu makali ya mwili, na malalamiko ya watu wa ukoo na marafiki zake, na wakati alipokabiliwa na kifo, mwenendo wake halisi kwa mara nyingine tena ulionyesha kimo chake kwa mambo yote.

Asili Halisi ya Ayubu: Mkweli, Aliyetakaswa, na Asiye na Uongo

Hebu tusome Ayubu 2:7-8: “Hivyo Shetani akatoka mbele za uwepo wa Yehova, na akamgonga Ayubu kwa majipu ya kuuma kutoka kwenye wayo wa mguu wake hadi utosini mwa kichwa chake. Na akachukua kigae kwa ajili ya kujikuna nacho; naye akakaa chini kwenye majivu.” Huu ni ufafanuzi wa mwenendo wa Ayubu wakati ambapo majipu yawashayo yalipoota kwenye mwili wake. Wakati huu, Ayubu aliketi kwenye majivu huku akiyavumilia. Hakuna aliyemtibu yeye, na hakuna aliyemsaidia kupunguza maumivu kwenye mwili wake; badala yake, alitumia kigaye cha chungu kukwaruza sehemu ya juu ya majipu yake yenye maumivu. Juu juu, hii ilikuwa awamu tu ya mateso ya Ayubu na haina uhusiano wowote na ubinadamu wake na kumcha Mungu kwake, kwani Ayubu hakuongea maneno yoyote kuonyesha hali na maoni yake wakati huo. Lakini matendo na mwenendo wake Ayubu bado ni onyesho la kweli la ubinadamu

wake. Kwenye rekodi za sura ya awali tunasoma kwamba Ayubu alikuwa ndiye mkuu zaidi kati ya wanaume wote wa mashariki. Kifungu hiki cha sura ya pili, nacho, kinatuonyesha kwamba binadamu huyu mkuu wa mashariki hakika alichukua kigae cha chungu na kujikwaruza nacho huku akiwa ameketi kwenye jivu. Je, hakuna ulinganuzi wowote wa wazi kati ya fafanuzi hizi mbili? Ni ulinganuzi unaotonyesha nafsi ya kweli ya Ayubu: Licha ya nafasi na hadhi yake ya kifahari, hakuwahi kuzipenda wala kuzitilia maanani yoyote; hakujali namna wengine walivyoangalia nafasi yake wala kuhusu kama hatua au mwenendo wake ungekuwa na athari mbaya kwa nafasi yake; hakujihusisha katika utajiri wa hali, wala hakufurahia utukufu uliokuja pamoja na hadhi na nafasi yake katika jamii. Alijali tu kuhusu thamani yake na umuhimu wa kuishi kwake mbele ya macho ya Yehova Mungu. Nafsi ya kweli ya Ayubu ilikuwa kiini chake: Hakupenda umaarufu na utajiri, na wala hakuishi kwa ajili ya umaarufu na utajiri; alikuwa mkweli, na aliyetakaswa, na aliye bila ya uongo wowote.

Utenganisho wa Ayubu kati ya Upendo na Chuki

Upande mwingine wa ubinadamu wa Ayubu unaonyeshwa katika mazungumzo yake na mke wake: “Kisha mkewe akasema kwake, Je, Wewe bado unabaki na ukamilifu wako? mlaani Mungu, ufe. Lakini yeye akasema kwake, Wewe unazungumza mithili ya mmoja wa wanawake walio wapumbavu wanavyozungumza. Ati? tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” (Ayubu 2:9-10). Kuona mateso aliyokuwa akipitia, mke wa Ayubu alijaribu kumshauri Ayubu ili amsaidie kutoroka mateso yake—lakini zile “nia nzuri” hazikupata idhini ya Ayubu; badala yake, ziliamsha ndani yake hasira, kwani alikataa imani yake katika na utiifu wake kwa Yehova Mungu na pia akakataa uwepo wa Yehova Mungu. Hali hii isingeweza kuvumilika kwa Ayubu, kwani hakuwahi kujiruhusu kufanya chochote ambacho kingepinga au kingemdhuru Mungu, bila kusema chochote kuhusu wengine. Angewezaje kubakia vilevile bila kujali chochote wakati alipowaona wengine wakiongea maneno yaliyomkufuru na kumtukana Mungu? Hivyo basi akamuita mke wake “mwanamke mjinga.” Mwelekeo wa Ayubu kwa mke wake ulikuwa ule wa hasira na chuki, pamoja na ule wa kushutumu na kukemea. Haya ndiyo yaliyokuwa maonyesho ya kiasili ya ubinadamu wa Ayubu ambayo yalitofautisha kati ya upendo na chuki na yalikuwa uwakilishi wa kweli wa ubinadamu wake uliokuwa na unyofu. Ayubu alimiliki hali fulani ya haki—hali ambayo ilimfanya kuchukua upepo na mawimbi ya maovu, na kumfanya kuchukua, kushutumu, na kukataa uzushi wa ajabu, mabishano ya kijinga na madai yasiyokuwa na msingi, na ikamruhusu kushikilia kanuni zake sahihi, za kweli kwake yeye mwenyewe na msimamo ule aliochukua wakati alipokuwa amekataliwa na wengi na kuachwa na wale walio kuwa karibu na yeye.

Ukarimu na Uaminifu wa Ayubu

Kwa sababu, kutoka katika mwenendo wa Ayubu, tunaweza kuona maonyesho ya vipengele mbalimbali vya ubinadamu wake, tunauona ubinadamu wa Ayubu upi anapokifunua kinywa chake kuilaani siku aliyojaliwa? Hii ndiyo mada tutakayozungumzia hapa chini.

Hapo juu, Nimezungumzia asili ya laana la Ayubu ya siku ya kuzaliwa kwake. Mnaona nini katika haya? Kama Ayubu asingekuwa mkarimu na asiye na upendo, kama angekuwa mnyama na asiye na hisia, na mpungufu wa ubinadamu, angejali kuhusu tamatio la moyoni mwa Mungu? Na je angedharau siku ya kuzaliwa kwake kutokana na kuutunza moyo wa Mungu? Kwa maneno mengine kama Ayubu alikuwa hana ukarimu na aliyepongukwa na ubinadamu, angedhikishwa na maumivu ya Mungu? Angeilaani siku yake ya kuzaliwa kwa sababu Mungu alikuwa amedhulumiwa na yeye? Jibu ni, bila shaka la! Kwa sababu alikuwa mkarimu, Ayubu aliutunza moyo wa Mungu; kwa sababu aliutunza moyo wa Mungu, Ayubu alihisi maumivu ya Mungu; kwa sababu alikuwa mkarimu, alipata maumivu makali zaidi kutokana na kuyahisi maumivu ya Mungu; kwa sababu aliyahisi maumivu ya Mungu, alianza kuichukia siku ya kuzaliwa kwake, na hivyo akailaani siku yake ya kuzaliwa. Kwa watu wa nje, mwenendo wote wa Ayubu wakati wa majaribio yake ni wa kupigiwa mifano. Kulaani kwake tu kwa siku ya kuzaliwa ndiko kunakoweka picha ya kiulizo juu ya utimilifu na unyofu wake, au kutoa utathmini tofauti. Kwa hakika, haya ndiyo yaliyokuwa maonyesho ya kweli zaidi ya kiini cha ubinadamu wa Ayubu. Kiini cha ubinadamu wake hakikufichwa au kubadilishwa, au kuduruswa na mtu mwingine. Alipoilaani siku yake ya kuzaliwa, alionyesha ukarimu na uaminifu uliokuwa ndani ya moyo wake; alikuwa kama chemichemi ya maji ambayo maji yake yalikuwa safi sana na angavu kiasi cha kufichua sehemu ya chini kabisa ya chemichemi hio.

Baada ya kujifunza haya yote kuhusu Ayubu, watu wengi zaidi bila shaka watakuwa na utathmini sahihi kwa kiasi fulani na usiopendelea kuhusu kiini cha ubinadamu wa Ayubu. Wanafaa pia kuwa na uelewa na kina kikuu cha kimatendo, na uliopevuka zaidi wa utimilifu na unyofu wa Ayubu kama ulivyozungumzwa na Mungu. Ni tumaini langu kwamba, uelewa na kina hiki kitawasaidia watu kuanza kushughulikia njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu.

Uhusiano Kati ya Mungu kumpa Shetani Ayubu na Malengo ya Kazi ya Mungu

Ingawaje watu wengi sasa wanatambua kwamba Ayubu alikuwa mtimilifu na mnyofu na kwamba alimcha Mungu na kujiepusha na maovu, utambuzi huu hauwapi uelewa mkubwa zaidi wa nia ya Mungu. Wakati huohuo wakionea wivu ubinadamu na ushughulikaji wa Ayubu, wanamuuliza Mungu swali lifuatalo: Ayubu alikuwa mtimilifu na mnyofu sana, watu walimpenda sana, kwa hivyo kwa nini Mungu akamkabidhi kwa Shetani na kumpitishia maumivu haya makali? Maswali kama hayo yanatarajiwa kuwepo katika mioyo ya watu wengi—

au, kushuku huku ndiko hasa swali katika mioyo ya watu wengi. Kwa sababu kushuku huku kumeshangaza watu wengi sana, lazima tuliwasilishe swali hili waziwazi na kulielezea kikamilifu.

Kila kitu ambacho Mungu anafanya kinahitajika, na kina umuhimu usio wa kawaida, kwani kila kitu anachofanya ndani ya binadamu kinahusu usimamizi wake na wokovu wa wanadamu. Kiasili kazi ambayo Mungu alimfanyia Ayubu si tofauti, ingawaje Ayubu alikuwa mtimilifu na mnyofu mbele ya macho ya Mungu. Kwa maneno mengine, licha ya kile ambacho Mungu anafanya au mbinu ambazo Anatumia kufanya, licha ya gharama, au lengo Lake, kusudio la hatua Zake halibadiliki. Kusudio Lake ni kuweza kumshughulikia binadamu ili maneno ya Mungu yaingie ndani yake, mahitaji ya Mungu, na mapenzi ya Mungu kwa binadamu; kwa maneno mengine, ni kufanyia kazi huyu binadamu ili vyote ambavyo Mungu Anasadiki kuwa vizuri kulingana na hatua Zake, kumwezesha binadamu kuuelewa moyo wa Mungu na kufahamu kiini cha Mungu, na kumruhusu yeye kutii ukuu na mipangilio ya Mungu, na hivyo basi kumruhusu binadamu kuweza kufikia kiwango cha kumcha Mungu na kujiepusha na maovu—yote ambayo ni kipengele kimoja ya kusudio la Mungu katika kila kitu Anachofanya. Kipengele kingine ni kwamba, kwa sababu Shetani ndiye foili na chombo cha huduma katika kazi ya Mungu, mara nyingi binadamu hukabidhiwa Shetani; hizi ndizo mbinu ambazo Mungu hutumia ili kuwaruhusu watu kuweza kuona maovu, ubaya, kudharaulika kwa Shetani katikati ya majaribio na mashambulizi ya Shetani na hivyo basi kuwasababisha watu kumchukia Shetani na kuweza kutambua kile ambacho ni kibaya. Mchakato huu unawaruhusu kwa utaratibu kuanza kuwa huru dhidi ya udhibiti wa Shetani, na dhidi ya mashtaka, uingiliaji kati, na mashambulizi ya Shetani—mpaka, kwa sababu ya maneno ya Mungu, maarifa yao na utiifu wao kwa Mungu, na imani yao kwa Mungu na kuweza kwao kumcha Mungu, wanashinda dhidi ya mashambulizi ya Shetani na kushinda dhidi ya mashtaka ya Shetani; hapo tu ndipo watakapokuwa wamekombolewa kabisa dhidi ya utawala wa Shetani. Ukombozi wa watu unamaanisha kwamba Shetani ameshindwa, unamaanisha kwamba wao si tena chakula kwenye kinywa cha Shetani—kwamba badala ya kuwameza wao, Shetani amewaachilia. Hii ni kwa sababu watu kama hao ni wanyofu, kwa sababu wanayo imani, utiifu na wanamcha Mungu, na kwa sababu wako huru kabisa dhidi ya Shetani. Wamemletea Shetani aibu, wamemfanya kuonekana mjinga, na wamemshinda kabisa Shetani. Imani yao katika kumfuata Mungu, na utiifu na kumcha Mungu kunamshinda Shetani, na kumfanya Shetani kukata tamaa kabisa na wao. Watu kama hawa ndio ambao Mungu amewapata kwa kweli, na hili ndilo lengo kuu la Mungu katika kumwoko binadamu. Kama wangependa kuokolewa, na wangependa Mungu awapate kabisa, basi wote wanaomfuata Mungu lazima wakabiliane na majaribio na mashambulizi yakiwa makubwa na hata madogo kutoka kwa Shetani. Wale wanaoibuka katika majaribio na mashambulizi haya na

wanaweza kumshinda Shetani ni wale waliookolewa na Mungu. Hivi ni kusema kwamba wale waliookolewa na Mungu ni wale ambao wamepitia majaribio ya Mungu, na ambao wamejaribiwa na kushambuliwa na Shetani mara nyingi. Wale waliookolewa na Mungu wanayaelewa mapenzi na mahitaji ya Mungu, na wanaweza kuukubali ukuu na mipangilio ya Mungu na hawaachi njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu katikati ya majaribio ya Shetani. Wale waliookolewa na Mungu wanamiliki uaminifu, wao ni wakarimu, na wanaweza kutofautisha upendo na chuki, wanayo hisia ya haki na urazini, na wanaweza kumtunza Mungu na kuthamini sana kila kitu ambacho ni cha Mungu. Watu kama hao hawatekwi bakunja, kufanyiwa upelelezi, kushtakiwa au kudhulumiwa na Shetani; wako huru kabisa, wamekombolewa na kuachiliwa kabisa. Ayubu alikuwa mtu kama huyo mwenye uhuru na huu ndio umuhimu hasa wa kwa nini Mungu alikuwa amemkabidhi kwa Shetani.

Ayubu alidhulumiwa na Shetani, lakini pia aliweza kupata uhuru na ukombozi wa milele, na kupata haki ya kutowahi kukabidhiwa tena kwa upotovu, unyanyasaji, na mashtaka ya Shetani, na badala yake kuishi katika nuru ya udhhibiti wa Mungu usio na pingamizi na kuishi katikati ya baraka kutoka kwa Mungu. Hakuna ambaye angechukua au kuangamiza, au kupata haki hii. Ilipewa kwa Ayubu kutokana na imani, bidii, na utiifu wake kwa na kumcha Mungu; Ayubu alilipia gharama ya maisha yake ili kuweza kupata shangwe na furaha duniani, ili kufanikiwa kupata haki na kuweza kustahili, kama ilivyoamriwa mbinguni na kutambuliwa na dunia, ili kumwabudu Muumba bila ya uingiliaji kati kama kiumbe wa kweli wa Mungu duniani. Hivyo pia ndivyo yalivyokuwa matokeo makubwa zaidi ya majaribio yaliyovumiliwa na Ayubu.

Wakati watu bado hawajaokolewa, maisha yao mara nyingi yanaingiliwa kati na hata kudhibitiwa na, Shetani. Kwa maneno mengine, watu ambao hawajaokolewa ni wafungwa wa Shetani, hawana uhuru, hawajaachiliwa na Shetani, hawajafuzu wala kustahili kumwabudu Mungu, na wanafuatiliwa kwa karibu na kushambuliwa kwa ukali na Shetani. Watu kama hawa hawana furaha ya kuzungumzia, hawana haki ya uwepo wa kawaida wa kuzungumzia, na zaidi hawana heshima ya kuzungumzia. Ni pale tu unaposimama imara na kupigana na Shetani, kwa kutumia imani yako katika Mungu na utiifu kwake, pamoja na kumcha Mungu kama silaha ambazo utatumia kupigana vita vya maisha na mauti dhidi ya Shetani, kiasi cha kwamba utamshinda kabisa Shetani na kumsababisha kukata tamaa na kuwa mwoga kila anapokuona wewe, ili aache kabisa mashambulizi na mashtaka yake dhidi yako—hapo tu ndipo utakapookolewa na kuwa huru. Kama umeamua kutengana kabisa na Shetani lakini huna silaha zitakazokusaidia kupigana na Shetani, basi bado utakuwa katika hatari; kwa kadri muda unaposonga, baada ya wewe kuteswa na Shetani kiasi cha kwamba huna hata usuli wa nguvu uliobakia ndani mwako, lakini bado hujaweza kuwa na ushuhuda, bado hujajifungua kabisa kuwa huru dhidi ya mashtaka na mashambulizi ya Shetani dhidi yako, basi utakuwa na tumaini

dogo la wokovu. Mwishowe, wakati hitimisho la kazi ya Mungu itakapotangazwa, bado utakuwa katika mashiko ya Shetani, usiweze kujiachilia kuwa huru, na hivyo hutawahi kuwa na fursa au tumaini. Matokeo yake, hivyo basi, ni kwamba watu kama hao watakuwa mateka kabisa wa Shetani.

Kubali Mitihani ya Mungu, Shinda Majaribio ya Shetani, na Mruhusu Mungu Kupata Nafsi Yako Nzima

Wakati wa kazi wa utoaji Wake wa kudumu na msaada kwa binadamu, Mungu anaambia binadamu kuhusu mapenzi Yake na mahitaji Yake yote, na anaonyesha vitendo Vyake, tabia, na kile Anacho na alichwa kwa binadamu. Lengo ni kuweza kumtayarisha binadamu ili awe na kimo, na kumruhusu binadamu kupata ukweli mbalimbali kutoka kwa Mungu wakati anaendelea kumfuata Yeye—ukweli ambao ni silaha alizopewa binadamu na Mungu ambazo atatumia kupigana na Shetani. Hivyo akiwa na silaha hizo, binadamu lazima akabiliane na mitihani ya Mungu. Mungu anazo mbinu na njia nyingi za kumjaribu binadamu, lakini kila mojawapo inahitaji “ushirikiano” wa adui wa Mungu: Shetani. Hivi ni kusema, baada ya kumpa binadamu silaha ambazo atatumia kupigana na Shetani, Mungu anamkabidhi binadamu kwa Shetani na kuruhusu Shetani “kujaribu” kimo cha binadamu. Kama binadamu anaweza kufanikiwa dhidi ya uundaji wa vita vya Shetani, kama anaweza kutoroka mizunguko ya Shetani na bado akaishi, basi mwanadamu atakuwa ameupita mtihani. Lakini kama binadamu atashindwa kuondoka kwenye uundaji wa vita vya Shetani, na kujinyenyekeza kwa Shetani, basi hatakuwa ameupita mtihani. Haijalishi ni kipengele kipi cha binadamu ambacho mungu anachunguza, kigezo cha uchunguzi Wake ni kama binadamu atasimama imara katika ushuhuda wake atakaposhambuliwa na Shetani au la, kujua kama amemuacha Mungu au la na akajisalimisha na akajinyenyekeza kwa Shetani baada ya kunaswa na Shetani. Inaweza kusemekana kwamba, iwapo binadamu anaweza kuokolewa au la yote haya yanategemea kama anaweza kumzidi na kumshinda Shetani, na kama ataweza kupata uhuru au la yanategemea kama anaweza kuinua, yeye binafsi, silaha alizopewa na Mungu ili kushinda utumwa wa Shetani, na kumfanya Shetani kuwacha kabisa tumaini na kumwacha pekee. Kama Shetani ataliacha tumaini na kumwachilia mtu, hii inamaanisha kwamba Shetani hatawahi tena kujaribu kuchukua mtu huyu kutoka kwa Mungu hatawahi tena kumshtaki na kuingilia kati mtu huyu, hatawahi tena kutaka kumtesa au kumshambulia; mtu kama huyu tu ndiye atakuwa kwa kweli amepatwa na Mungu. Huu ndio mchakato mzima ambao Mungu anapata watu.

Onyo na Nuru Iliyotolewa kwa Vizazi vya Baadaye Na Ushuhuda wa Ayubu

Huku wakielewa mchakato ambao Mungu anampata kabisa mtu, watu wataweza pia kuelewa nia na umuhimu wa Mungu kumpeleka Ayubu kwa Shetani. Watu hawasumbuliwi tena

na maumivu makali ya Ayubu, na wanatambua upya umuhimu wake. Hawawi na wasiwasi tena kuhusu kama wao wenyewe watapitia majaribio sawa na yale ya Ayubu, na hawapingi tena au kukataa tena ujio wa majaribio ya Mungu. Imani, utiifu, na ushuhuda wake Ayubu wa kushinda Shetani, vyote hivi vimekuwa ni chanzo cha msaada mkubwa na himizo kwa watu. Kwa Ayubu, wanaona tumaini la wokovu wao binafsi, na wanaona kwamba kupitia kwa imani na utiifu kwa na kumcha Mungu, inawezekana kabisa kushinda Shetani, na kumshinda Shetani. Wanaona kwamba mradi tu waukubali ukuu na mipangilio ya Mungu, na kumiliki uamuzi na imani ya kutomwacha Mungu baada ya kupoteza kila kitu, basi wanaweza kumletea Shetani aibu na hali ya kushindwa, na kwamba wanahitaji tu kumiliki uamuzi na ustahimilivu wa kusimama imara katika ushuhuda wao—hata kama itamaanisha kupoteza maisha yao—ili Shetani aweze kuaibika na kurejea nyuma haraka. Ushuhuda wa Ayubu ni onyo kwa vizazi vya baadaye, na onyo hili linawaambia kwamba kama hawatamshinda Shetani, basi hawatawahi kuweza kujiondolea mashtaka na uingiliaji kati wa Shetani, na wala hawatawahi kuweza kutoroka dhulma na mashambulizi ya Shetani. Ushuhuda wa Ayubu ulipatia nuru vizazi vya baadaye. Upatiaji Nuru huu unafunza watu kwamba ni pale tu wanapokuwa watimilifu na wanyofu ndipo watakapoweza kumcha Mungu na kujiepusha na maovu; unawafunza kwamba ni pale tu wanapomcha Mungu na kujiepusha na maovu ndipo watakapoweza kuwa na ushuhuda wenye udhabiti na wa kipekee kwa Mungu; pale tu watakapokuwa na ushuhuda dhabiti na wakipekee wa Mungu ndipo hawatawahi kudhibitiwa na Shetani, na kuishi katika mwongozo na ulinzi wa Mungu—na hapo tu ndipo watakapokuwa wameokolewa kwa kweli. Hulka ya Ayubu na ufuatiliaji wake wa maisha unafaa kuigwa na kila mmoja anayefuata wokovu. Kile alichioishi kwa kudhihirisha katika maisha yake yote na mwenendo wake wakati wa majaribio yake ni hazina yenye thamani kwa watu wote wanaotaka kufuata njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu.

Ushuhuda wa Ayubu Wamliwaza Mungu

Nikiwaambia sasa kwamba Ayubu ni mtu mzuri, huenda msiweze kutambua maana iliyo katika maneno haya, na huenda msiweze kung'amua mawazo yaliyofanya Nizungumze maneno haya yote; lakini subirini mpaka siku ile mtakapokuwa mmepitia majaribu sawa na au yale yanayofanana na yale ambayo Ayubu alipitia, wakati mtakapokuwa mmepitia magumu, wakati mtakapokuwa mmepitia majaribu yaliyopangiliwa kwa ajili yenu na Mungu mwenyewe, wakati utakapojitolea kila kitu ulicho nacho, na kuvumilia udhalilishaji na ugumu ili uweze kumshinda Shetani na kuwa na ushuhuda kwa Mungu katikati ya vishawishi hivi vyote—basi utaweza kutambua maana ya maneno haya Ninayoyaongea. Wakati huo, utahisi kwamba wewe ni duni kuliko Ayubu, utahisi namna Ayubu alivyo mzuri na kwamba anastahili kuigwa; wakati huo utakapowadia, utatambua namna ambavyo maneno yale yaliyo bora yaliyozungumzwa na Ayubu yalivyo muhimu kwa yule aliyepotoka na anayeishi katika nyakati hizi, na utatambua namna

ilivyo vigumu kwa watu wa leo kuweza kutimiza kile ambacho Ayubu alitimiza. Unapohisi kuwa ni vigumu, utatambua na kuona namna ambavyo moyo wa Mungu una dukuduku na wasiwasi, utatambua namna gharama aliyolipa Mungu kuwapata watu kama hao ilivyo ya juu, na jinsi kile ambacho Mungu hufanya na kutumia kwa ajili ya mwanadamu kilivyo cha thamani. Kwa sababu sasa mmeyasikia maneno haya, je, mnao ufahamu sahihi na ukadiriaji wa kweli kuhusu Ayubu? Machoni penu, je, Ayubu alikuwa kweli mtu mtimilifu na mnyofu aliyemcha Mungu na kujiepusha na maovu? Nasadiki kwamba watu wengi bila shaka watasema ndiyo. Kwani ukweli kuhusu kile ambacho Ayubu alitenda na kufichua hakiwezi kupingwa na binadamu yeyote au Shetani. Hivyo ndivyo thibitisho la nguvu zaidi kuhusu ushindi wa Ayubu dhidi ya Shetani. Thibitisho hili lilitolewa katika Ayubu, na ndio ushuhuda wa kwanza uliopokelewa na Mungu. Hivyo, Ayubu aliposhinda vishawishi vya Shetani na kuwa na ushuhuda kwa Mungu, Mungu aliona tumaini kwake Ayubu, na moyo wake uliliwazwa na Ayubu. Tangu wakati wa uumbaji mpaka wakati wa Ayubu, huu ndio ulikuwa wakati wa kwanza ambao Mungu kwa kweli alipitia na kujua kuliwazwa kulikuwa nini, na kuliwazwa na mwanadamu kulimaanisha nini. Huo ndio ulikuwa wakati wa kwanza ambao Alikuwa ameona, na kupata ushuhuda wa kweli uliotokana na Yeye.

Ninaamini kwamba, baada ya kuusikia ushuhuda wa Ayubu na simulizi za vipengele mbalimbali vya Ayubu, watu wengi watakuwa na mipango ya njia iliyo mbele yao. Hivyo, pia, Ninaamini kwamba watu wengi zaidi walio na wasiwasi na woga wataanza kwa utaratibu kuwa watulivu katika mwili na akili zao, na wataanza kuhisi tulizo, hatua kwa hatua ...

Vifungu vilivyo hapa chini ni simulizi pia kumhusu Ayubu. Acha tuendelee kusoma.

4. Ayubu Asikia Kuhusu Mungu Kupitia Kusikiliza kwa Sikio

Ayubu 9:11 Ona, Anapita karibu na mimi, na Simwoni: Anapita kwenda mbele pia, lakini siwezi kumwona.

Ayubu 23:8-9 Tazama, nasonga mbele, lakini hayuko huko; na nyuma, lakini siwezi kumwona: Kwa mkono wa kushoto, ambapo Yeye hufanya kazi, lakini siwezi kumwona: Yeye hujificha Mwenyewe katika mkono wa kulia, kiasi kwamba siwezi kumwona.

Ayubu 42:2-6 Najua ya kwamba Wewe unaweza kufanya kila kitu, na ya kwamba hakuna wazo linaloweza kuzuilika kutoka Kwako. Ni nani yeye anayeficha ushauri bila maarifa? hivyo, nimesema neno nisilolifahamu; vitu vilivyo vya ajabu sana kwangu, ambavyo nisivyovijua. Sikiza, nakusihi, nami nitazungumza: Nitautiliza kutoka Kwako, Nawe useme kwangu. Nimesikia kukuhusu kwa kusikia na masikio: lakini sasa jicho langu lakuona. Ndiyo sababu najichukia, na kutubu kwenye mavumbi na majivu.

Ingawa Mungu Hajajifichua kwa Ayubu, Ayubu Anauamini Ukuu wa Mungu

Nguvu za maneno haya ni nini? Je, Yupo yeyote aliyetambua kwamba kuna ukweli hapa? Kwanza, ni vipi ambavyo Ayubu alijua kwamba Mungu yupo? Kisha, ni vipi alivyojua kwamba mbingu na ardhi na mambo yote yanatawaliwa na Mungu? Kunacho kifungu kinachojibu maswali haya mawili: “Nimesikia kukuhusu kwa kusikia na masikio: lakini sasa jicho langu lakuona. Ndiyo sababu najichukia, na kutubu kwenye mavumbi na majivu” (Ayubu 42:5-6). Kutokana na maneno haya tunajifunza kwamba, badala ya kumwona Mungu kwa macho yake mwenyewe, Ayubu alikuwa amejifunza kuhusu Mungu kutoka kwa hekaya. Ni katika hali hizi ndipo alipoanza kuitembea njia ya kumfuata Mungu, na baadaye akathibitisha uwepo wa Mungu katika Maisha yake, na kati ya mambo yote. Kuna ukweli usiopingika hapa—ukweli huo ni upi? Licha ya kuweza kufuata njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, Ayubu alikuwa hajawahi kumwona Mungu. Katika haya, hakuwa sawa na watu wa leo? Ayubu alikuwa hajawahi kumwona Mungu, matokeo yake ni kwamba ingawa alikuwa amewahi kumsikia Mungu, hakujua ni wapi Mungu alikuwa, au ni vipi Mungu alifanana, au ni nini ambacho Mungu alikuwa akifanya. Haya yote ni mambo ambayo ni ya kibinafsi; tukiongea bila mapendeleo, ingawa alimfuata Mungu, Mungu alikuwa hajawahi kumwonekana yeye au kumzungumzia yeye. Je, huu si ukweli? Ingawa Mungu alikuwa hajaongea na Ayubu au kumpa amri zozote, Ayubu alikuwa ameuona uwepo wa Mungu na kutazama ukuu Wake miongoni mwa mambo yote, na katika hekaya ambazo kwazo Ayubu alikuwa amesikia kumhusu Mungu kwa kusikia kwa sikio, na baadaye alianza maisha ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Hizi ndizo zilizokuwa asili na mchakato ambao Ayubu alimfuata Mungu. Lakini haikujalisha ni vipi alivyomcha Mungu na kujiepusha na maovu, ni vipi ambavyo alishikilia uadilifu wake, bado Mungu alikuwa hajawahi kujitokeza kwake. Hebu tukisome kifungu hiki. Alisema, “Ona, Anapita karibu na mimi, na simwoni: Anapita kwenda mbele pia, lakini siwezi kumwona” (Ayubu 9:11). Yale ambayo maneno haya yanasema ni kwamba Ayubu huenda alihisi Mungu karibu naye au pengine hakuhisi—lakini alikuwa hajawahi kuweza kumwona Mungu. Kunazo nyakati ambapo alifikiria Mungu akipita mbele yake au akitenda, au akimwongoza binadamu, lakini alikuwa hajawahi kujua. Mungu humjia binadamu wakati ambapo hatarajii; binadamu hajui ni lini Mungu atamjia, au ni wapi anapomjia yeye, kwa sababu binadamu hawezi kumwona Mungu, kwa hivyo, kwa binadamu Mungu amejificha kutoka kwake.

Imani ya Ayubu Katika Mungu Haitikisiki Kwa Sababu ya Ukweli Kwamba Mungu Amejificha Kutoka Kwake

Katika kifungu kifuatacho cha maandiko, Ayubu anasema, “Tazama, nasonga mbele, lakini Hayuko huko; na nyuma, lakini siwezi kumwona: Kwa mkono wa kushoto, ambapo Yeye

hufanya kazi, lakini siwezi kumwona: Yeye hujificha katika mkono wa kulia, kiasi kwamba siwezi kumwona” (Ayubu 23:8-9). Katika simulizi hii, tunajifunza kwamba katika hali alizopitia Ayubu, Mungu alikuwa Amejificha kutoka kwake wakati wote huo; Mungu alikuwa hajajitokeza waziwazi kwake, na alikuwa hajamzungumzia waziwazi maneno yoyote, lakini katika moyo wake Ayubu alikuwa na ujasiri wa uwepo wa Mungu. Alikuwa siku zote ameamini kwamba Mungu huenda anatembea na yeye au huenda Anatenda akiwa kando yake, na kwamba ingawa hakuweza kumwona Mungu, Mungu alikuwa kando yake Akitawala mambo yote kumhusu yeye. Ayubu alikuwa hajawahi kumwona Mungu, lakini aliweza kuwa mkweli katika imani yake, jambo ambalo hakuna mtu yeyote aliwahi kuweza kufanya. Kwa nini watu wengine wasiweze kufanya hivyo? Ni kwa sababu Mungu hakuongea na Ayubu au kumwonekana, na asingekuwa ameamini kwa kweli, asingeweza kuendelea, wala asingeweza kushikilia njia hiyo ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Je, huu si ukweli? Unahisi vipi unaposoma kumhusu Ayubu akisema maneno haya? Unahisi kwamba utimilifu na unyofu wa Ayubu, na haki yake mbele ya Mungu, ni kweli, na wala si kupiga chuku kwa upande wa Mungu? Ingawa Mungu alimshughulikia Ayubu kwa njia sawa na watu wengine, na hakujitokeza wala kuongea na yeye, Ayubu bado alishikilia uadilifu wake, bado aliamini ukuu wa Mungu, na, isitoshe, mara kwa mara alitoa sadaka za kuteketezwa na kuomba mbele ya Mungu kutokana na hofu yake ya kumkosea Mungu. Katika uwezo wa Ayubu wa kumcha Mungu bila ya kuwahi kumwona Mungu, tunaona ni kiasi kipi alichopenda mambo mazuri na ni vipi imani yake ilivyokuwa thabiti na ya kweli. Hakukana uwepo wa Mungu kwa sababu Mungu alikuwa amejificha kutoka kwake, wala hakupoteza imani yake na kumkataa Mungu kwa sababu hakuwahi kumwona Yeye. Badala yake, katikati ya kazi fiche ya Mungu ya kutawala mambo yote, alikuwa ametambua uwepo wa Mungu na akahisi ukuu wa Mungu na Nguvu za Mungu. Hakukata tamaa katika kuwa mnyofu kwa sababu Mungu alikuwa amejificha, wala hakuiacha njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu kwa sababu Mungu alikuwa hajawahi kumwonekana. Ayubu alikuwa hajawahi kuuliza kwamba Mungu aonekane waziwazi kwake ili kuthibitisha uwepo Wake, kwani alikuwa tayari ametangaza ukuu wa Mungu miongoni mwa mambo yote na aliamini kwamba alikuwa amepata baraka na neema ambazo wengine hawakuwa wamepata. Ingawa Mungu alibakia amejificha kutoka kwake, imani ya Ayubu kwa Mungu haikuwahi kutikisika. Hivyo, alivuna kile ambacho hakuna yeyote aliwahi kuvuna. Kibali cha Mungu na baraka za Mungu.

Ayubu Alibariki Jina la Mungu na Hafikirii Baraka au Janga

Kunao ukweli ambao haurejelewi katu kwenye hadithi za maandiko kuhusu Ayubu, na ukweli huu ndio utakaokuwa lengo letu leo. Ingawa Ayubu alikuwa hajawahi kumwona Mungu au kusikia maneno ya Mungu kwa masikio yake mwenyewe, Mungu alikuwa na nafasi katika moyo wa Ayubu. Mtazamo wa Ayubu kwa Mungu ulikuwa upi? Ulikuwa, kama ulivyorejelewa

awali, “jina la Yehova libarikiwe.” Baraka yake kwa jina la Mungu haikuwa ya masharti, pasipo kujali muktadha, na bila kushurutishwa na sababu yoyote. Tunaona kwamba Ayubu alikuwa ameukabidhi moyo wake kwa Mungu, na kuuruhusu udhibitiwe na Mungu; kila kitu alichofikiria, kila kitu alichoaamua, na kila kitu alichopanga katika moyo wake kilikuwa wazi kwa Mungu na wala moyo wake haukuwa umefungwa kuzuia Mungu. Moyo wake haukumpinga Mungu, na hakuwahi kuuliza Mungu kumfanyia chochote au kumpa chochote yeye, na wala hakuwa na matamano yasiyo ya kawaida kwamba angepata chochote kutokana na yeye kumwabudu Mungu. Ayubu hakuzungumzia mabadilishano na Mungu, na wala hakutoa ombi lolote au madai yoyote kwa Mungu. Kulisifu kwake jina la Mungu kulikuwa kwa sababu ya nguvu kuu na mamlaka ya Mungu katika kutawala mambo yote, na haikutegemea kama alipata baraka au alipigwa na janga. Aliamini kwamba haijalishi kama Mungu anawabariki watu au analeta janga kwao, mamlaka na nguvu vyote havitabadilika, na hivyo, haikujalisha hali za mtu, jina la Mungu linafaa kusifiwa. Kwamba binadamu amebarikiwa na Mungu ni kwa sababu ya ukuu wa Mungu, na janga linapompata mwanadamu, hivyo, pia ni kwa sababu ya ukuu wa Mungu. Nguvu na mamlaka ya Mungu vyote vinatawala na kupangilia kila kitu kumhusu mwanadamu; matukio yasiyo ya kawaida kuhusu utajiri wa binadamu ni maonyesho ya nguvu na mamlaka ya Mungu, na licha ya maoni yake mtu, jina la Mungu linafaa kusifiwa. Haya ndiyo ambayo Ayubu alipitia na kuishia kujua katika miaka ya maisha yake. Fikiria na matendo yote ya Ayubu vyote vilifikia masikio ya Mungu na vikawasili mbele ya Mungu, na vikaonekana kuwa muhimu na Mungu. Mungu aliyapenda sana maarifa haya ya Ayubu na akamthamini sana Ayubu kwa kuwa na moyo kama huo. Moyo huu ulisubiria amri ya Mungu siku zote, na pahali pote, na haijalishi ni muda au mahali gani palipokaribisha chochote kile kilichomsibu. Ayubu hakutoa mahitaji yoyote kwa Mungu. Kile alichohitaji kutoka kwake kilikuwa kusubiria, kukubali, kukabiliana na kutii mipangilio yote iliyotoka kwa Mungu; Ayubu aliamini hili kuwa wajibu wake, na ndicho hasa kile ambacho Mungu Alitaka. Ayubu alikuwa hajawahi kumwona Mungu wala kumsikiliza Akiongea mambo yoyote, akitoa amri zozote, akiyoa mafundisho yoyote, au kumwelekeza kuhusu chochote. Kwa maneno ya leo, yeye kuweza kumiliki mtazamo kama huo kwa Mungu, wakati Mungu alikuwa hajampa nuru, mwongozo, au toleo kuhusiana na ukweli— hili lilikuwa lenye thamani sana, na kwake yeye kuonyesha mambo kama hayo kulitoshwa kwa Mungu, na ushuhuda wake ulipongezwa na Mungu, na kutunzwa na Mungu. Ayubu alikuwa hajawahi kumwona Mungu au kumsikia Mungu binafsi akitamka mafundisho yoyote kwake yeye, lakini kwa Mungu moyo wake na yeye mwenyewe vyote vilikuwa vyenye thamani zaidi kuliko wale watu ambao, mbele ya Mungu waliweza tu kuongea kuhusiana na nadharia kuu, ambao waliweza tu kujigamba na kuongea kuhusu kutoa sadaka lakini walikuwa hawajawahi kuwa na maarifa ya kweli ya Mungu na walikuwa hawajawahi kumcha Mungu kwa kweli. Kwa kuwa moyo wa Ayubu ulikuwa safi, na haukufichwa kuonekana na Mungu, na ubinadamu wake

ulikuwa wenye uaminifu na ukarimu, na alipenda haki na kile kilichokuwa kizuri. Binadamu kama huyu pekee aliyemiliki moyo kama huo na ubinadamu ndiye aliyeweza kufuata njia ya Mungu, na kuwa na uwezo wa kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Binadamu kama huyo angeona ukuu wa Mungu, angeona mamlaka na nguvu Yake, na angeweza kutimiza utiifu kwa ukuu Wake na mipangilio. Binadamu tu kama huyo ndiye angeweza kulisifu jina la Mungu kwa kweli. Hii ni kwa sababu hakuangalia kama Mungu angembariki au Angemletea janga, kwa sababu alijua kwamba kila kitu kinadhibitiwa na mkono wa Mungu, na kwamba binadamu kuwa na wasiwasi ni ishara ya ujinga, kutojua, na kutoweza kufikiria vyema, kuwa na shaka kuhusu ukweli wa ukuu wa Mungu juu ya mambo yote, na ya kutomcha Mungu. Maarifa ya Ayubu hasa ndiyo ambayo Mungu alitaka. Hivyo basi, Ayubu alikuwa na maarifa makubwa ya kinadharia kumhusu Mungu kuliko ninyi? Kwa sababu kazi na matamko ya Mungu wakati huo yalikuwa machache, halikuwa jambo rahisi kutimiza maarifa ya Mungu. Mafanikio kama hayo ya Ayubu hayakuwa jambo dogo. Alikuwa hajapitia kazi ya Mungu wala kuwahi kumsikia Mungu akiongea, au kuuona uso wa Mungu. Kwamba aliweza kuwa na mtazamo kama huo kwa Mungu yalikuwa hasa matokeo ya ubinadamu wake na ufuatiliaji wake binafsi, ubinadamu na ufuatiliaji ambao watu hawana leo. Hivyo, katika enzi hiyo, Mungu alisema, “Hakuna mtu ambaye yuko kama yeye ulimwenguni, mtu aliye mkamilifu na mwaminifu.” Katika enzi hiyo, Mungu alikuwa tayari amefanya ukadiriaji wa aina hiyo kumhusu Ayubu, na Alikuwa amefikia hitimisho kama hilo. Ungekuwa ukweli zaidi kwa kiasi kipi hii leo?

Ingawa Mungu Amejificha Kutoka kwa Mwanadamu, Matendo Yake Miongoni mwa Mambo Yote Yanatosha Binadamu Kumjua Yeye

Ayubu alikuwa hajauona uso wa Mungu, wala kusikia matamshi yaliyoongelewa na Mungu, na sembuse yeye kuipitia kazi ya Mungu, lakini kumcha kwake Mungu na ushuhuda aliokuwa nao wakati wa majaribu unashuhudiwa na kila mmoja, na unapendwa, unafurahiwa, na kupongezwa na Mungu na watu wanayaonea wivu na kuvutiwa nayo, na hata zaidi ya hayo, wanaimba sifa zao. Hakukuwepo chochote kikubwa au kisicho cha kawaida kuhusu maisha yake: Kama vile tu mtu yeyote wa kawaida, aliishi maisha yasiyo ya kina, akienda kufanya kazi wakati wa macheo na akirudi nyumbani kupumzika wakati wa magharibi. Tofauti ni kwamba wakati wa miongo mbalimbali ya maisha yake isiyo ya ajabu, alipata maono kuhusu njia ya Mungu, na akatambua na kuelewa nguvu kubwa na ukuu wa Mungu kuliko mtu yeyote mwingine. Hakuwa mwerevu zaidi kuliko mtu yeyote wa kawaida, maisha yake hayakuwa sanasana yenye ushupavu, wala, aidha, yeye hakuwa na mbinu maalum zisizoonekana. Kile alichomiliki, hata hivyo, kilikuwa ni hulka iliyokuwa na uaminifu, upole na unyofu, na hulka iliyopenda kutopendelea, haki, na iliyopenda mambo chanya—hakuna kati ya mambo haya yanayomilikiwa na watu wengi wa kawaida. Alitofautisha kati ya upendo na chuki, alikuwa na

hisia ya haki, hakukubali kushindwa na alikuwa hakati tamaa, na alikuwa mwangalifu sana katika kufikiria kwake. Hivyo, wakati wake usio wa ajabu duniani aliyaona mambo yote yasiyo ya kawaida ambayo Mungu alikuwa amefanya, na aliuona ukubwa, utakatifu, na kuwa na haki kwa Mungu, aliona kujali kwa Mungu, neema yake, na ulinzi wake wa binadamu, na aliuona utukufu na mamlaka ya Mungu mkuu zaidi. Sababu ya kwanza iliyomfanya Ayubu aweze kupata mambo haya yaliyokuwa zaidi ya mtu yeyote wa kawaida ilikuwa kwamba alikuwa na moyo safi, na moyo wake ulimilikiwa na Mungu na kuongozwa na Muumba. Sababu ya pili ilikuwa ni ufuatiliaji wake: ufuatiliaji wake wa kuwa maasumu na mtimilifu, na wa kuwa mtu aliyekubaliana na mapenzi ya Mbinguni, aliyependwa na Mungu, na aliyejiepisha na uovu. Ayubu alimiliki na kufuatilia mambo haya huku akiwa hawezi kumwona Mungu au kusikia maneno ya Mungu; ingawa alikuwa hajawahi kumwona Mungu, alikuwa amejua mbinu ambazo kwazo Mungu alitawala mambo yote, na kuelewa hekima ambayo Mungu anatumia ili kufanya hivyo. Ingawa alikuwa hajawahi kusikia maneno ambayo yalikuwa yametamkwa na Mungu, Ayubu alijua kwamba matendo ya kutuza binadamu na kuchukua kutoka kwa binadamu yote yalitoka kwa Mungu. Ingawa miaka ya maisha yake haikuwa tofauti na ile ya mtu wa kawaida, hakuruhusu kutokuwa wa ajabu kwa maisha yake kuathiri maarifa yake ya ukuu wa Mungu juu ya mambo yote, au kuathiri kufuata kwake kwa njia za kumcha Mungu na kujiepisha na maovu. Machoni pake, sheria za mambo yote zilizaa matendo ya Mungu na ukuu wa Mungu ungeweza kuonekana katika sehemu yoyote ya maisha ya mtu. Hakuwa amemwona Mungu lakini aliweza kutambua kwamba Matendo ya Mungu yako kila pahali, na katika wakati wake usiokuwa wa ajabu duniani, katika kila kona ya maisha yake aliweza kuona na kutambua matendo ya kipekee na ya maajabu ya Mungu, na aliweza kuona mipangilio ya ajabu ya Mungu. Ufiche na kimya cha Mungu havikuzuia utambuzi wa Ayubu wa matendo ya Mungu, wala havikuathiri maarifa yake kuhusu ukuu wa Mungu juu ya mambo yote. Maisha yake yalikuwa utambuzi, katika maisha yake ya kila siku, wa ukuu na mipangilio ya Mungu, ambaye Amejificha miongoni mwa mambo yote. Katika maisha yake ya kila siku alisikia pia na kuelewa sauti ya moyo wa Mungu na maneno ya Mungu, akiwa kimya miongoni mwa mambo yote lakini anaonyesha sauti ya moyo Wake na maneno kwa kutawala sheria ya mambo yote. Unaona, basi, kwamba kama watu wanao ubinadamu sawa na ufuatiliaji kama Ayubu, basi wanaweza kupata utambuzi na maarifa sawa kama Ayubu, na kupata ule ufahamu na maarifa sawa kuhusu ukuu wa Mungu juu ya mambo yote kama Ayubu. Mungu hakuwa amemwonekana Ayubu au kuongea na yeye, lakini Ayubu aliweza kuwa mtimilifu na mnyofu, na pia aliweza kumcha Mungu na kujiepisha na maovu. Kwa maneno mengine, bila ya Mungu kumwonekana au kuongea na binadamu, matendo ya Mungu miongoni mwa mambo yote na ukuu Wake juu ya mambo yote yanatosha kwa mwanadamu ili kuweza kuwa na ufahamu wa uwepo, nguvu na mamlaka ya Mungu, nguvu na mamlaka ya Mungu yanatosha kumfanya mwanadamu afuate njia ya kumcha Mungu na

kujiepusha na maovu. Kwa sababu mwanadamu wa kawaida kama vile Ayubu aliweza kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, basi kila mtu wa kawaida anayemfuata Mungu anafaa pia kuweza kufanya hivyo. Ingawa maneno haya yanaweza kusikika kana kwamba ni hitimisho la kimantiki, hili halikiuki sheria ya mambo. Bado ukweli haujalingana na matarajio: Kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, kunaweza kuonekana, ni hifadhi ya Ayubu na Ayubu pekee. Kwa kutaja “kumcha Mungu na kujiepusha na maovu,” watu hufikiri kwamba hii inafaa tu kufanywa na Ayubu, ni kana kwamba njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu ilikuwa imebandikwa jina la Ayubu na haikuhusiana na watu wengine. Sababu ya hili ni wazi: Kwa sababu Ayubu tu ndiye aliyemiliki hulka iliyokuwa na uaminifu, ukarimu, na unyofu, na iliyopenda kutopendelea na haki na mambo yaliyokuwa mazuri, hivyo ni Ayubu tu ambaye angeweza kufuata njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Lazima nyinyi nyote muwe mmeelewa matokeo hapa—kwa sababu hakuna yule anayemiliki ubinadamu ulio na uaminifu, ukarimu, na unyofu, na ule ambao unapenda kutopendelea na haki na ule ambao ni mzuri, hakuna mtu anayeweza kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, na hivyo watu hawawezi kamwe kupata furaha ya Mungu au kusimama imara katikati ya majaribu. Hii pia inamaanisha kwamba, bila kujumuisha Ayubu, watu wote wangali wamefungwa na kutegwa na Shetani; wote wanashtakiwa, wanashambuliwa, na kudhulumiwa na yeye. Wao ndio wale ambao Shetani anajaribu kumeza, na wote hawana uhuru, ni wafungwa ambao wametekwa nyara na Shetani.

Kama Moyo wa Mwanadamu Una Uadui na Mungu, Mwanadamu Anawezaje Kumcha Mungu na Kujiepusha na Maovu?

Kwa sababu watu wa leo hawamiliki ubinadamu sawa na Ayubu, sembuse kiini cha asili yao, na mtazamo wao kwa Mungu? Wanamcha Mungu? Wanajiepusha na maovu? Wale wasiomcha Mungu na kujiepusha na maovu wanaweza kujumuishwa tu kwa maneno matatu: “adui wa Mungu.” Mara nyingi ninyi husema maneno haya matatu, lakini hamjawahi kujua maana yake halisi. Maneno “ni adui wa Mungu” yanayo kiini ndani yake: Hayasemi kwamba Mungu anamuona mwanadamu kama adui, lakini kwamba binadamu anamuona Mungu kama adui. Kwanza, watu wanapoanza kumwamini Mungu, ni yupi kati yao asiyekuwa na nia, motisha na tabia yake binafsi ya makuu? Ingawa sehemu moja yao inaamini uwepo wa Mungu, na imeona uwepo wa Mungu, imani yao katika Mungu bado ina hiyo motisha, na nia yao kuu ya kumwamini Mungu ni kupokea baraka Zake na vitu wanavyotaka. Katika uzoefu wa watu katika maisha yao, mara nyingi wao hufikiria, nimetoa familia yangu na ajira yangu kwa Mungu, na Amenipa nini? Lazima niongezee na kuthibitisha haya—je, nimepokea baraka zozote hivi majuzi? Nimetoa mengi sana wakati huu, nimekimbia na kukimbia na kuteseka sana—je, Mungu amenipa ahadi zozote baada ya haya? Je, Amekumbuka matendo yangu mazuri? Mwisho wangu utakuwa vipi? Ninaweza kuzipokea baraka za Mungu? ... Kila mtu kila wakati hufanya hesabu

kama hizi ndani ya moyo wake, na yeye hutoa madai yake kwa Mungu yanayoonyesha motisha yake, malengo na mawazo ya mabadilishano. Hii ni kusema, ndani ya moyo wake mwanadamu siku zote humweka Mungu majaribuni, siku zote anaunda njama kumhusu Mungu, akijitetea kwa Mungu kila wakati kwa sababu ya mwisho wake binafsi na kujaribu kumfanya Mungu atoe kauli, aweze kuona kama Mungu anaweza kumpa kile anachotaka au la. Wakati huohuo akimfuata Mungu, binadamu hamchukulii Mungu kama Mungu. Siku zote mwanadamu amejaribu kufanya mipango na Mungu, akitoa madai bila kusita kwake Yeye na hata akimsukuma Yeye katika kila hatua, akijaribu kupiga hatua ya maili licha ya kupewa inchi moja. Wakati huohuo akijaribu kufanya mabadilishano na Mungu, binadamu pia anabishana na Yeye, na wapo hata watu ambao, wakati majaribu yanawapata au wanapojipata katika hali ya kuteketea, mara nyingi wanakuwa wanyonge, wananyamaza na kuzembea katika kazi yao, na wanajaa malalamiko kumhusu Mungu. Tangu wakati ambapo mwanadamu alianza kumwamini Mungu, amemchukulia Mungu kama alama ya pembe inayoonyesha wingi wa neema, kisu cha Kijeshi cha Uswisi, na amejichukulia yeye mwenyewe kuwa mdaiwa mkubwa zaidi wa Mungu, ni kana kwamba kujaribu kupata baraka na ahadi kutoka kwa Mungu ni haki na jukumu lake la asili, huku jukumu la Mungu likiwa ni kumlinda na kumtunza mwanadamu na kumruzuku. Huu ndio ufahamu wa kimsingi wa “imani katika Mungu” wa wale wote wanaomwamini Mungu, na ufahamu wao wa kina zaidi wa dhana ya imani katika Mungu. Kutoka katika kiini cha asili ya mwanadamu hadi katika ufuatiliaji wake wa kibinafsi, hakuna kitu chochote kinachohusiana na kumcha Mungu. Nia ya mwanadamu katika kumwamini Mungu huenda isiwe na uhusiano na kumwabudu Mungu. Hivi ni kusema kwamba, mwanadamu hajawahi kufikiria wala kuelewa kwamba imani katika Mungu inahitaji kumcha Mungu, na kumwabudu Mungu. Kwa mujibu wa haya yote, kiini cha mwanadamu kiko wazi. Kiini hiki ni kipi? Ni kwamba moyo wa mwanadamu ni mwovu, unaficha udanganyifu na ujanja, haupendi mambo ya kutopendelea na haki na kile kilicho chanya, nao ni wenye kustahili dharau na ulafi. Moyo wa mwanadamu umemfungia Mungu nje sana, hajampa Mungu moyo wake kabisa. Mungu hajawahi kuona moyo wa kweli wa mwanadamu, wala hajawahi kuabudiwa na mwanadamu. Haijalishi jinsi gharama ambayo Mungu amelipia ilivyo kubwa, au ni kiasi kipi cha kazi Anachofanya, au ni kiwango kipi Anachompa mwanadamu, mwanadamu anabakia yule asiyeona hayo yote, na hajali kuyahusu. Mwanadamu hajawahi kumpa Mungu moyo wake, anataka tu kuujali moyo wake yeye mwenyewe, kufanya uamuzi wake mwenyewe—sababu ikiwa kwamba mwanadamu hataki kufuata njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, au kutii ukuu na mipangilio ya Mungu, wala hataki kumwabudu Mungu kama Mungu. Hivyo ndivyo hali ya mwanadamu ilivyo leo. Sasa hebu tumwangalie tena Ayubu. Kwanza kabisa, je, alifanya mabadilishano na Mungu? Je, alikuwa na nia zozote fiche katika kushikilia njia ile ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu? Wakati huo, je, Mungu alikuwa ameongea na yeyote kuhusu

mwisho unaokuja? Wakati huo, Mungu alikuwa hajatoa ahadi zozote kwa yeyote kuhusu mwisho, na ilikuwa katika hali hii ndipo Ayubu aliweza kumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Je, watu wa leo wanaweza kulinganishwa na Ayubu? Kunazo tofauti nyingi sana; wamo katika viwango tofauti. Ingawa Ayubu hakuwa na maarifa mengi ya Mungu, alikuwa amempa Mungu moyo wake na ulimilikiwa na Mungu. Hakuwahi kufanya mabadilishano na Mungu, na hakuwa na matamano yoyote ya kupita kiasi au madai kwa Mungu; badala yake, aliamini kwamba “Yehova alinipa, na Yehova amechukua.” Hiki ndicho alikuwa ameona na kupata kutokana na kushikilia njia ya kumcha Mungu kwa uaminifu na kujiepusha na maovu katika miaka yake mingi ya maisha. Vivyo hivyo, alikuwa pia amepata matokeo yanayowakilishwa katika maneno: “Nasi tupokee mema kutoka mkononi mwa Mungu, nasi tusipokee mabaya?” Sentensi hizi mbili ndizo ambazo alikuwa ameona na akaja kujua kutokana na mtazamo wake wa utiifu kwa Mungu katika uzoefu wa maisha yake, na ndizo pia zilikuwa silaha zake zenye nguvu zaidi ambazo alitumia kushinda wakati wa vishawishi vya Shetani, na ndizo zilikuwa msingi wa kusimama kwake imara katika ushuhuda kwa Mungu. Wakati huu, je, bado mnamwona Ayubu kama mtu mzuri? Je, mnatumaini kuwa mtu kama huyo? Je, mnaogopa kupitia vishawishi vya Shetani? Je, mnaamua kumwomba Mungu ili aweze kuwapitisha katika majaribu kama haya ya Ayubu? Bila shaka watu wengi wasingethubutu kuomba mambo kama hayo. Ni wazi, basi, kwamba imani yenu ni ndogo kiasi cha kusikitisha; ikilinganishwa na ile ya Ayubu, imani yenu haistahili kutajwa. Nyinyi ndio adui wa Mungu, hamumchi Mungu, hamwezi kusimama imara katika ushuhuda kwa Mungu, na hamwezi kuyashinda mashambulio, mashtaka, na vishawishi vya Shetani. Ni nini kinachowafanya mstahili kupokea ahadi za Mungu? Baada ya kusikia hadithi ya Ayubu na kuelewa nia ya Mungu katika kumwokoia mwanadamu na maana ya wokovu wa mwanadamu, je, sasa mna imani ya kukubali majaribu sawa na ya Ayubu? Je, hampaswi kuwa na kusudio kidogo mjiruhusu kufuata njia ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu?

Msiwe na Wasiwasi Wowote Kuhusu Majaribio ya Mungu

Baada ya kuupokea ushuhuda kutoka kwa Ayubu kufuatia mwisho wa majaribio yake, Mungu aliamua kwamba angepata kundi au zaidi ya kundi—la watu kama Ayubu, ilhali aliamua kutowahi tena kumruhusu Shetani kushambulia au kunyanyasa mtu yeyote mwingine kwa kutumia mbinu ambazo kwazo alimjaribu, kumshambulia na kumnyanyasa Ayubu, kwa kufanya mzaha na Mungu; Mungu hakumruhusu Shetani tena kufanya mambo kama hayo kwa binadamu ambaye ni mnyonge, mjinga, na asiyejua—ilikuwa tosha kwamba Shetani alikuwa amemjaribu Ayubu! Kutomruhusu Shetani kuwanyanyasa watu vyovyote anavyotaka ndiyo rehema ya Mungu. Kwa Mungu, ilitosha kwamba Ayubu alikuwa ameteseka majaribio na minyanyaso ya Shetani. Mungu hakumruhusu Shetani tena kufanya mambo kama hayo, kwani maisha na kila kitu cha watu wanaomfuata Mungu yanatawaliwa na kupangiliwa na Mungu, na Shetani hastahili

kutawala waliochaguliwa na Mungu apendavyo—mnafaa kuwa wazi kuhusu hoja hii! Mungu anajali kuhusu unyonge wa binadamu, na kuelewa ujinga na kutojua kwake. Ingawaje, ili binadamu aweze kuokolewa kabisa, lazima Mungu amkabidhi kwa Shetani, Mungu hayuko radhi kumwona tena binadamu akichezewa kama mjinga na kunyanyaswa na Shetani na hataki kumwona binadamu siku zote akiteseka. Binadamu aliumbwa na Mungu, na inaeleweka kikamilifu kwamba Mungu anatawala na anapangilia kila kitu cha binadamu; hili ni jukumu la Mungu na mamlaka ambayo Mungu anatawala mambo yote! Mungu hamruhusu Shetani kunyanyasa na kutumia vibaya binadamu apendavyo, Hamruhusu Shetani kutumia mbinu mbalimbali za kumpotosha binadamu, na vilevile, Hamruhusu Shetani kuingilia kati ukuu wa Mungu kwa binadamu, wala Hamruhusu Shetani kukanyaga na kuangamiza Sheria ambazo Mungu anatawalia mambo yote, kutosema chochote kuhusu kazi kuu ya Mungu ya kusimamia na kuwaokoa wanadamu! Wale ambao Mungu anataka kuokoa na wale ambao wanaweza kuwa na ushuhuda kwa Mungu, ndio msingi na hali halisi ya kazi ya Mungu ya mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita, pamoja na bei ya jitihada zake katika kazi yake ya miaka elfu sita. Mungu anawezaje kuwakabidhi watu hawa kwa Shetani hivihivi.

Watu mara nyingi wanakuwa na wasiwasi kuhusu na wana uoga wa majaribio ya Mungu, ilhali siku zote wanaishi katika mtego wa Shetani na kuishi katika maeneo hatari ambapo wanashambuliwa na kunyanyaswa na Shetani—lakini hawaogopi na hawashangazwi. Nini kinaendelea? Imani ya binadamu katika Mungu ni finyu mno kwa mambo anayoweza kuona. Hana shukrani hata chembe kuhusu upendo na kujali kwa Mungu kwa binadamu, au wema Wake na utiliaji maanani kwa binadamu. Lakini kwa hofu na wasiwasi kidogo kuhusu majaribio, hukumu na kuadibu kwa Mungu na adhama na hasira Yake, binadamu hana hata chembe cha uelewa wa nia nzuri za Mungu. Kwa kutajwa kwa majaribio, watu wanahisi ni kana kwamba Mungu anazo nia nyingine zisizo wazi na hata baadhi wanasadiki kwamba Mungu ana mipango ya maovu, wasijue hata kile ambacho Mungu atawafanyia; hivyo, wakati huohuo kutaka kuwa watiifu kabisa kwa ukuu na mipangilio ya Mungu, wanafanya kila wawezalo kuzuia na kupinga ukuu wa Mungu juu ya binadamu na mipangilio kwa binadamu, kwani wanasadiki kwamba kama hawatakuwa makini watapotoshwa na Mungu, na kama hawatakuwa na mshikilio thabiti wa hatima yao binafsi, basi kila kitu walicho nacho kinaweza kuchukuliwa na Mungu, na maisha yao huenda hata yakaisha. Binadamu yumo kwenye kambi la Shetani, lakini hawi na wasiwasi kamwe kuhusu kunyanyaswa na Shetani, na ananyanyaswa na Shetani lakini haogopi kamwe kutekwa nyara na Shetani. Siku zote anasema kwamba anaukubali wokovu wa Mungu, ilhali hajawahi kumwamini Mungu au kusadiki kwamba Mungu atamwokoa kwa kweli kutoka kwenye makucha ya Shetani. Kama, sawa na Ayubu, binadamu anaweza kunyenyekea kwa mipango na mipangilio ya Mungu na anaweza kuitoa nafsi nzima kwa mikono ya Mungu, basi hatima ya

binadamu haitakuwa sawa na ile ya Ayubu—kupokea baraka za Mungu? Kama binadamu anaweza kukubali na kunyenyekea Sheria ya Mungu, nini kipo cha kupoteza? Na hivyo Napendekeza kwamba muwe makinifu kwa vitendo vyenu, mtahadhari na kila kitu ambacho kiko karibu kuwafanyikia ninyi. Usiwe wa pupa au msukumo na umshughulikie Mungu na watu, masuala, vitu alivyokupangilia kwa namna mshawasha unavyokupeleka, au kulingana na nafsi yako ya kiasili au kufikiria na dhana zako; lazima uwe makini katika vitendo vyako na lazima uombe na utafute zaidi, kuepuka kuchochea hasira ya Mungu. Kumbuka hili!

Kisha, tutaangalia vile Ayubu alikuwa baada ya majaribio yake.

5. Ayubu Baada ya Majaribio Yake

Ayubu 42:7-9 Na basi ikawa, kwamba baada ya Yehova kusema maneno haya kwa Ayubu, Yehova akasema kwa Elifazi Mtemani, Ghadhabu yangu inawaka dhidi yako, na dhidi ya hao marafiki zako wawili: kwa sababu nyinyi hamjasema kunihusu kile kilicho sawa, jinsi alivyofanya mtumishi Wangu Ayubu. Kwa hivyo sasa, jichukulieni ng’ombe wa kiume saba, na kondoo wa kiume saba, na muende kwake mtumishi Wangu Ayubu, na mjitolee sadaka ya kuteketezwa; na mtumishi Wangu Ayubu atawaombea: kwa kuwa yeye nitamkubali: Nisije nikawatendea kulingana na makosa yenu, hivi kwamba nyinyi hamkusema kunihusu kile kilicho sawa, kama alivyofanya mtumishi Wangu Ayubu. Hivyo Elifazi Mtemani, na Bildadi Mshuhi, na Sofari Mnaamathi, wakaenda, na kufanya vile Yehova alivyowaamrisha: Yehova pia akamkubali Ayubu.

Ayubu 42:10 Naye Yehova akaubadilisha uteka wa Ayubu, wakati alipowaombea marafiki zake: Yehova pia akampa Ayubu kiasi kilichozidishwa mara mbili kuliko yale aliyokuwa nayo awali.

Ayubu 42:12 Kwa hivyo Yehova akabariki Ayubu zaidi baadaye maishani kuliko mwanzo wake: kwa sababu alikuwa na kondoo elfu kumi na nne, na ngamia elfu sita, na elfu moja ya jozi za ng’ombe, na elfu moja ya punda wa kike.

Ayubu 42:17 Kwa hivyo Ayubu akafariki, akiwa mzee na aliyejawa na siku.

Wale Wanaomcha Mungu na Kujiepusha Na Maovu Wanatazamiwa kwa Utunzwaji na Mungu, Huku Wale Walio Wajinga Wanaonekana kuwa Duni na Mungu

Katika Ayubu 42:7-9, Mungu Anasema kwamba Ayubu ni mtumishi Wake. Matumizi Yake ya neno “mtumishi” kumrejelea Ayubu yanaonyesha umuhimu wa Ayubu katika moyo Wake; ingawaje Mungu hakumwita Ayubu kitu chenye heshima zaidi, jina hili halikuwa na uamuzi wowote katika umuhimu wa Mungu ndani ya moyo wa Ayubu. “Mtumishi” hapa ni jina la

lakabu la Mungu kwa Ayubu. Marejeleo mengi ya Mungu kwa “mtumishi Wangu Ayubu” yanaonyesha ni vipi ambavyo Alipendezwa na Ayubu, ingawaje Mungu hakuongea kuhusu maana ya nyuma ya neno “Mtumishi,” ufafanuzi wa Mungu wa neno “mtumishi” unaweza kuonekana kupitia kwa maneno Yake katika kifungu hiki cha maandiko. Kwanza Mungu alimwambia Elifazi Mtemani: “Ghadhabu yangu inawaka dhidi yako, na dhidi ya hao marafiki zako wawili: kwa sababu nyinyi hamjasema kunihusu kile kilicho sawa, jinsi alivyofanya mtumishi Wangu Ayubu.” Maneno haya ndiyo ya mara ya kwanza kwa Mungu kuambia watu waziwazi kwamba alikuwa amekubali yale yote yaliyokuwa yamesemwa na kufanywa na Ayubu baada ya majaribio ya Mungu kwake yeye, na ndiyo mara ya kwanza Alikuwa amethibitisha waziwazi ukweli na usahihi wa yale yote Ayubu alikuwa amefanya na kusema. Mungu alikuwa na ghadhabu kwake Elifazi na wengine kwa sababu ya mazungumzo yao yasiyokuwa sahihi na mabovu, kwa sababu, kama Ayubu wasingeweza kuona mwonekano wa Mungu au kusikia maneno aliyoongea katika maisha yao ilhali Ayubu alikuwa na maarifa sahihi Kumhusu Mungu, huku nao waliweza tu kukisia bila mpango kuhusu Mungu, kukiuka mapenzi ya Mungu na kujaribu uvumilivu wake kwa yote waliyoyafanya. Kwa hivyo, wakati sawa na kukubali yote yalikuwa yamefanywa na kusemwa na Ayubu, Mungu alizidi kuongeza hasira zake kwa wale wengine, kwani ndani yao Hakuweza tu kuuona uhalisia wowote wa kumcha Mungu, lakini pia Hakusikia chochote cha kumcha Mungu kwa yale waliyoyasema. Na hivyo Mungu kwa kilichofuata Alisema madai yafuatayo kuwahusu. “Kwa hivyo sasa, jichukulieni ng’ombe wa kiume saba, na kondoo wa kiume saba, na muende kwake mtumishi wangu Ayubu, na mjitolee sadaka ya kuteketezwa; na mtumishi wangu Ayubu atawaombea: kwa kuwa yeye nitamkubali: nisije nikawatendea kulingana na makosa yenu.” Katika kifungu hiki Mungu anamwambia Elifazi na wengine kufanya jambo ambalo litakomboa dhambi zao, kwani upumbavu wao ulikuwa ni dhambi dhidi ya Yehova Mungu, na hivyo wangelazimika kutoa sadaka zilizoteketezwa ili kusuluhisha makosa yao. Sadaka zilizoteketezwa mara nyingi zinatolewa kwa Mungu, lakini kile kisicho cha kawaida kuhusu sadaka hizi zilizoteketezwa ni kwamba zilitolewa kwa Ayubu. Ayubu alikubaliwa na Mungu kwa sababu alikuwa nao ushuhuda kwa Mungu wakati wa majaribio yake. Rafiki hawa wa Ayubu, nao walifichuliwa katika kipindi kile cha majaribio yake, kwa sababu ya upumbavu wao, walishutumiwa na Mungu na wakachochea hasira ya Mungu, na wanafaa kuadhibiwa na Mungu—kuadhibiwa kwa kutoa sadaka zilizoteketezwa mbele ya Ayubu—na baadaye Ayubu aliwaombea wao ili kuiondoa ile adhabu na hasira ya Mungu kwao. Nia ya Mungu ilikuwa ni kuwaaibisha wao, kwani hawakuwa watu waliomcha Mungu na wa kujiepusha na maovu, na walikuwa wameshutumu uadilifu wa Ayubu. Kwa upande mmoja, Mungu alikuwa akiwaambia kwamba Hakukubali vitendo vyao lakini Alikubali pakubwa na Alifurahishwa na Ayubu; kwa upande mwingine, Mungu alikuwa akiwaambia kwamba kukubaliwa na Mungu kunampandisha daraja binadamu mbele ya Mungu,

kwamba binadamu anachukiwa na Mungu kwa sababu ya upumbavu wake, na anamkosea Mungu kwa sababu ya hali hii, na anakuwa mdogo na mbaya mbele ya macho ya Mungu. Huu ndio ufafanuzi uliotolewa na Mungu kuhusu watu wa aina mbili, ni mielekeo ya Mungu kwa watu hawa wa aina mbili na ni ufafanuzi wa Mungu kuhusu thamani na hadhi ya watu wa aina hizi mbili. Ingawaje Mungu alimwita Ayubu mtumishi Wake, ndani ya macho ya Mungu huyu “mtumishi” alikuwa mpendwa Wake, na alipewa mamlaka ya kuwaombea wengine na kuwasamehe makosa yao. “Mtumishi huyu” aliweza kuongea moja kwa moja na Mungu na kuwa na mgusano wa moja kwa moja na Mungu, hadhi yake ilikuwa ya juu zaidi na ya heshima zaidi kuliko ya wale wengine. Haya ndiyo maana halisi ya neno “mtumishi” kama Mungu alivyoongea. Ayubu alipewa heshima hii maalum kwa sababu ya kumcha Mungu na kujiepusha na maovu, na sababu iliyofanya wengine kutoitwa watumishi na Mungu ni kwa sababu hawakumcha Mungu na kujiepusha na maovu. Mielekeo hii miwili tofauti na maalum ya Mungu ndiyo mielekeo yake kwa watu wa aina mbili: Wale wanaomcha Mungu na kujiepusha na maovu wanakubaliwa na Mungu, na wanaonekana wenye thamani mbele ya macho Yake, huku wale walio wapumbavu hawajamcha Mungu na hawawezi kujiepusha na maovu, na hawawezi kupokea kibali cha Mungu, mara nyingi wanachukiwa na kushutumiwa na Mungu, na ni wadogo mbele ya macho ya Mungu.

Mungu Anamtawaza Ayubu Mamlaka

Ayubu aliwaombea rafiki zake, na baadaye, kwa sababu ya maombi ya Ayubu, Mungu hakushughulika nao kama walivyostahili juu ya upumbavu wao—Hakuwaadhibu au kuchukua adhabu yoyote dhidi yao. Na sababu ilikuwa nini? Kwa sababu kulingana na wao maombi yanayohusu mtumishi wa Mungu, Ayubu, yalikuwa yamefikia masikio Yake; Mungu naye aliwasamehe kwa sababu Aliyakubali maombi ya Ayubu. Na tunaona nini katika haya? Wakati Mungu anapombariki mtu, Anampa tuzo nyingi, na si tu zile za kidunia: Mungu anawapa pia mamlaka, na Kuwaambia kuwa wanastahili kuwaombea wengine, naye Mungu husahau na kusamehe makosa ya hao watu kwa sababu Anayasikia maombi haya. Haya ndiyo mamlaka yenyewe ambayo Mungu alimpa Ayubu. Kupitia kwa maombi ya Ayubu kusitisha kushutumiwa kwao, Yehova Mungu aliwaletea aibu wale watu wapumbavu—ambayo, bila shaka, ndiyo iliyokuwa adhabu Yake maalum kwa Elifazi na wale wengine.

Ayubu Anabarikiwa kwa Mara Nyingine Tena na Mungu, na Hashtakiwi Tena na Shetani

Miongoni mwa matamko ya Yehova Mungu ni maneno kwamba “nyinyi hamkusema kunihusu kile kilicho sawa, kama alivyofanya mtumishi wangu Ayubu.” Ni nini kile ambacho Ayubu alikuwa amesema? Ni kile tulichozungumzia awali, pamoja na kile ambacho kurasa nyingi za maneno kwenye kitabu cha Ayubu ambacho Ayubu amerekodiwa kuwa alisema.

Katika kurasa hizi nyingi za maneno, Ayubu hajawahi hata mara moja kuwa na malalamiko au mashaka yoyote kumhusu Mungu. Yeye anasubiria tu matokeo. Ni kusubiri huku ambako ndiko mwelekeo wake wa uaminifu, matokeo yake yakiwa, na kutokana na maneno aliyomwambia Mungu, Ayubu alikubaliwa na Mungu. Alipovumilia majaribio na kupata mateso ya Ugumu, Mungu alikuwa upande wake na ingawaje ugumu wake hukupunguzwa na uwepo wa Mungu, Mungu aliona kile Alichotaka kuona na kusikia kile Alichotaka kusikia. Kila mojawapo ya vitendo na maneno ya Ayubu kiliweza kufikia macho na masikio ya Mungu; Mungu alisikia na Akaona—na hii ni ukweli. Maarifa ya Ayubu kumhusu Mungu na fikira zake kumhusu Mungu katika moyo wake wakati huo, katika kipindi hicho, hazikuwa kwa hakika kama zile za watu wa leo, lakini katika muktadha wa wakati huo, Mungu aliweza kutambua bado kila kitu alichokuwa amesema, kwa sababu tabia yake na fikira zake ndani ya moyo wake, na kile alichokuwa ameeleza na kufichua, kilikuwa tosha kwa mahitaji Yake. Katika kipindi hiki cha wakati ambao Ayubu alipitia majaribio, yale ambayo alifikiria katika moyo wake na kuamua kufanya yaliweza kumwonyesha Mungu matokeo, yale ambayo yalimtosheleza Mungu, na baadaye Mungu akayaondoa majaribio ya Ayubu, Ayubu akaibuka kutoka kwenye matatizo yake, na majaribio yake yakawa yameondoka yasiwahi kumpata tena yeye. Kwa sababu Ayubu alikuwa tayari amepitia majaribio, na akawa amesimama imara katika majaribio haya, na akamshinda kabisa Shetani, Mungu alimpatia baraka ambazo kwa kweli alistahili. Kama ilivyorekodiwa katika Ayubu 42:10, 12, Ayubu alibarikiwa kwa mara nyingine tena, na akabarikiwa zaidi ya hata mara ya kwanza. Wakati huu Shetani alikuwa amejiondoa, na hakusema tena au kufanya chochote, na kutoka hapo kuenda mbele Ayubu hakuhitilafiana tena na Shetani au kushambulia Shetani, na Shetani hakutoa mashtaka tena dhidi ya baraka za Mungu kwa Ayubu.

Ayubu Aishi Nusu ya Mwisho ya Maisha Yake Katikati ya Baraka za Mungu

Ingawaje baraka Zake wakati huo zilikuwa tu zinajumuisha kondoo, ng'ombe, ngamia, na rasilimali za dunia, na kadhalika, baraka ambazo Mungu alitaka kumpa Ayubu katika moyo Wake zilikuwa mbali zaidi na hizi. Kwa wakati huo ziliporekodiwa, ni aina gani za ahadi za milele ambazo Mungu alipenda kumpa Ayubu? Katika baraka Zake kwa Ayubu, Mungu hakugusia au kutaja kuhusu mwisho wake, na haijalishi umuhimu au cheo ambacho Ayubu alishikilia ndani ya moyo wa Mungu, kwa ujumla Mungu alikuwa mwangalifu sana katika baraka Zake. Mungu hakutangaza mwisho wa Ayubu. Hii inamaanisha nini? Wakati huo, wakati mpango wa Mungu ulikuwa bado haujafikia sehemu ya kutangaza mwisho wa binadamu, mpango huo ulikuwa bado uingie kwenye awamu ya mwisho ya kazi yake, Mungu hakutaja chochote kuhusu mwisho, huku akimpa binadamu baraka za rasilimali za dunia tu. Maana ya hii ni kwamba nusu ya mwisho ya maisha ya Ayubu ilipita katikati ya baraka za Mungu na hii ndiyo iliyomfanya kuwa tofauti na wale watu wengine—lakini kama wao alizeeka, na kama mtu yeyote

yule wa kawaida siku ilifika ambapo aliuambia ulimwengu kwaheri. Na hivyo imerekodiwa kwamba “Kwa hivyo Ayubu akafariki, akiwa mzee na aliyejawa na siku” (Ayubu 42:17). Nini maana ya “akafariki akiwa amejawa na siku” hapa? Katika enzi ya kabla Mungu kutangaza mwisho, Mungu alimwekea Ayubu matarajio ya maisha ambayo angeishi, na wakati umri huo ulipofikiwa Alimruhusu Ayubu kuondoka kiasili kutoka ulimwengu huu. Kutoka baraka ya pili ya Ayubu hadi kifo chake, Mungu hakuongezea ugumu wowote. Kwake Mungu, kifo cha Ayubu kilikuwa cha kiasili, na pia kilihitajika; kilikuwa kitu cha kawaida sana na wala si hukumu au shutuma. Alipokuwa hai, Ayubu alimwabudu na kumcha Mungu; kuhusiana na ni aina gani ya mwisho aliyokuwa nayo kufuatia kifo chake, Mungu hakusema chochote, wala kutoa maoni yoyote kuhusu hilo. Mungu ni mwenye utaratibu sana katika kile Anachosema na kufanya, na maudhui na kanuni za maneno na vitendo vyake yanalingana na awamu ya kazi Yake na kipindi Anachofanyia kazi. Ni aina gani ya mwisho ambayo mtu kama Ayubu alikuwa nayo katika moyo wa Mungu? Je, Mungu alikuwa amefikia aina yoyote ya uamuzi katika moyo Wake? Bila shaka Alikuwa! Ni vile tu hili lilikuwa halijulikani kwa binadamu; Mungu hakutaka kumwambia binadamu wala Hakuwa na nia yoyote ya kumwambia binadamu. Na hivyo, kwa kuongea juujuu tu, Ayubu alikufa akiwa amejawa na siku, na hivyo ndivyo maisha ya Ayubu yalivyokuwa.

Gharama Iliyoishi kwa kudhihirishwa na Ayubu Wakati wa Maisha Yake

Je, Ayubu aliishi maisha ya thamani? Thamani yake ilikuwa wapi? Ni kwa nini inasemwa kwamba aliishi maisha yenye thamani? Kwa binadamu, thamani yake ilikuwa gani? Kutoka katika mtazamo wa binadamu, aliwawakilisha wanadamu ambao Mungu alitaka kuokoa, kwa kuwa na ushuhuda wa kipekee kwa Mungu mbele ya Shetani na watu wa ulimwengu. Alitimiza wajibu ambao ulistahili kutimizwa na kiumbe wa Mungu, na kuweka mfano halisi wa kuigwa, na kutenda kama kielelezo, kwa wale wote ambao Mungu angependa kuwaokoa, akiruhusu watu kuona kwamba inawezekana kabisa kushinda Shetani kwa kumtegemea Mungu. Nayo thamani yake kwa Mungu ilikuwa gani? Kwa Mungu, thamani ya maisha ya Ayubu ilikuwa ndani ya uwezo wake wa kumcha Mungu, kumwabudu Mungu, kutolea ushuhuda vitendo vya Mungu, na kusifu vitendo vya Mungu, kumpa Mungu tulizo na kitu cha kufurahia; kwa Mungu, thamani ya maisha ya Ayubu ilikuwa pia kwa namna ambavyo, kabla ya kifo chake, Ayubu alipitia majaribio na kushinda Shetani, na akawa na ushuhuda wa kipekee kwa Mungu mbele ya Shetani na watu wa ulimwengu, akimtukuza Mungu miongoni mwa wanadamu, akiutuliza moyo wa Mungu na kuruhusu moyo wa Mungu wenye hamu kuyaona matokeo, na kuliona tumaini. Ushuhuda wake uliweka mfano wa kufuatwa kutokana na uwezo wake wa kusimama imara katika ushuhuda wa Mungu, na kuweza kumwaibisha Shetani kwa niaba ya Mungu, katika kazi ya Mungu ya kuwasimamia wanadamu. Je, hii si thamani ya maisha ya Ayubu? Ayubu alileta tulizo kwa moyo wa Mungu, alimpa Mungu kionjo cha furaha ya kutukuzwa, na akaanzisha

mwanzo mzuri kwa mpango wa usimamizi wa Mungu. Na kuanzia hapo kuenda mbele jina la Ayubu likawa ishara ya utukuzaji wa Mungu na ishara ya kushinda kwa wanadamu dhidi ya Shetani. Kile Ayubu aliishi kwa kudhihirisha wakati wa maisha yake na ushindi wake wa kipekee dhidi ya Shetani milele utabakia ukifurahiwa mno na Mungu na utimilifu wake, unyofu, na hali yake ya kumcha Mungu itaheshimiwa na kuigwa na vizazi vitakavyokuja. Milele atafurahiwa mno na Mungu kama johari lisilo na makosa, wala dosari, na pia ndivyo alivyo na thamani ya kuthaminiwa sana na binadamu!

Kisha, hebu tuangalie kazi ya Mungu wakati wa Enzi ya Sheria.

D. Taratibu za Enzi ya Sheria

Amri Kumi

Kanuni za Kujenga Madhabahu

Taratibu za Ushughulikiaji wa Watumishi

Taratibu za Wizi na Fidia

Kutimiza Mwaka wa Sabato na Karamu Tatu

Taratibu za Siku ya Sabato

Taratibu za Kutoa Sadaka

Sadaka zilizoteketezwa

Sadaka za Unga

Sadaka za Amani

Sadaka za Dhambi

Sadaka za Hatia

Taratibu za Sadaka za Kuhani (Aroni na Watoto Wake wa Kiume Waamrisha Kutii)

Sadaka za Kuteketezwa na Kuhani

Sadaka za Unga na Kuhani

Sadaka za Dhambi na Kuhani

Sadaka za Hatia na Kuhani

Sadaka za Amani na Kuhani

Taratibu za Ulaji wa Sadaka na Kuhani

Wanyama Walio Halali na Wale Walio Haramu (Wale Wanaoweza na Wasioweza Kuliwa)

Taratibu za Utakasaji Wanawake Baada ya Kujifungua

Viwango vya Uchunguzi wa Ukoma

Taratibu kwa Wale Ambao Wameponywa Ukoma

Taratibu za Kuzitakasa Nyumba Zilizoambukizwa

Taratibu za Wale Wanaougua Kisonono Kisicho cha Kawaida

Siku ya Upatanisho Wa Mungu na Binadamu Ambayo Lazima Iadhimishwe Mara Moja Kwa Mwaka

Sheria za Kuchinja Ng'ombe na Mbuzi

Kuzuiliwa kwa Mazoea Yafuatayo Yanayochukiza Ya Watu wa Mataifa (Si Kutenda Kujamiiiana Kwa Maharimu, na Kadhalika)

Taratibu Ambazo Lazima Zifuatwe na Watu (“Mtakuwa watakatifu: kwani Mimi Yehova Mungu wenu ni mtakatifu.”)

Kutendewa kwa Wale Wanaotoa Kafara Watoto Wao kwa Molka

Taratibu za Adhabu ya Uhalifu wa Uasherati

Sheria Zinazofaa Kufuatiliwa na Kuhani (Sheria za Tabia Yao Ya Kila Siku, Sheria za Matumizi ya Mambo matakatifu, Sheria za Kutoa Sadaka na Kadhalika)

Karamu Zinazofaa Kufuatiliwa (siku ya Sabato, Pentekoste, Siku ya Upatanisho wa Mungu na Binadamu kwa Maisha ya Kifo cha Yesu, na Kadhalika)

Taratibu Nyingine (Kuteketezwa kwa Taa, Mwaka wa Jubili, Ukombozi wa Ardhi, Ulaji wa Viapo, Utoaji wa Zaka, na Kadhalika)

Taratibu za Enzi ya Sheria ni Thibitisho la Kweli la Maelekezo ya Mungu kwa Wanadamu Wote

Hivyo, mmezisoma taratibu na kanuni hizi za Enzi ya Sheria, kweli? Je, taratibu hizi zinajumuisha mseto mpana? Kwanza, zinajumuisha Amri Kumi, na baadaye kuna taratibu za

namna ya kujenga madhabahu, na kadhalika. Hizi zinafuatwa na taratibu za kuitimiza Sabato na kuzidumisha zile karamu tatu, na baadaye kuna taratibu za kutoa sadaka. Je, mnaona ni aina ngapi za sadaka ambazo zimo? Kunazo sadaka zilizoteketezwa, sadaka za unga, sadaka za amani, sadaka za dhambi, na kadhalika. Zinafuatwa na taratibu za sadaka za kuhani, zikiwemo sadaka zilizoteketezwa na sadaka za unga zilizotolewa na Kuhani, na aina nyingine za sadaka. Taratibu za nane ni za ulaji wa sadaka na Kuhani. Na kisha kunazo taratibu zinazofaa kudumishwa wakati wa maisha ya watu. Kunayo masharti ya vipengele vingi vya maisha ya watu, kama vile taratibu zinazotawala kile wanachoweza au wasichoweza kula, kwa utakasaji wa wanawake baada ya wao kujifungua, na kwa wale ambao wameponywa ugonjwa wa ukoma. Katika taratibu hizi, Mungu Anafikia hadi kiwango cha kuzungumzia kuhusu ugonjwa, na kunazo hata sheria za kuchinja kondoo na ng'ombe, na kadhalika. Kondoo na ng'ombe waliumbwa na Mungu, na unafaa kuwachinja hata hivyo Mungu anakuambia kufanya hivyo; kunayo, bila shaka, sababu ya maneno ya Mungu, na ni sahihi bila shaka kutenda kama inavyokaririwa na Mungu, na kwa hakika itakuwa ya manufaa kwa watu! Kunazo pia karamu na sheria za kufuatwa, kama vile siku ya Sabato, Pasaka, na zaidi—Mungu aliweza kuzungumzia yote haya. Hebu tuangalie zile za mwisho: taratibu nyingine—kuteketezwa kwa taa, mwaka wa Jubilii, ukombozi wa ardhi, ulaji wa viapo, utoaji wa zaka, na kadhalika. Je, hizi zinajumuisha mseto mpana? Kitu cha kwanza cha kuzungumziwa ni suala la sadaka la watu, kisha kunazo taratibu za wizi na fidia, na udumishaji wa siku ya Sabato...; kila mojawapo ya maelezo ya maisha yanahusishwa. Hivi ni kusema, wakati Mungu alianza kazi Yake rasmi ya mpango Wake wa usimamizi, Aliweka wazi taratibu nyingi ambazo zilifaa kufuatwa na binadamu. Taratibu hizi zilikuwa ili kumruhusu binadamu kuishi maisha ya kawaida ya binadamu hapa duniani, maisha ya kawaida ya binadamu ambayo hayajatenganishwa na Mungu na uongozi Wake. Mungu alimwambia binadamu kwanza namna ya kuunda madhabahu, namna ya kuyaunda madhabahu. Baada ya hapo, Alimwambia binadamu namna ya kutoa sadaka, na kuamuru namna ambavyo binadamu alifaa kuishi—kile alichofaa kutilia maanani katika maisha, kile alichofaa kutii, kile anachofaa na hafai kufanya. Kile Mungu alichoweka wazi kwa binadamu kilikuwa kinakubalika chote, na pamoja na tamaduni, taratibu, na kanuni hizi Aliwastanisha tabia ya watu, kuongoza maisha yao, kuongoza uanzishaji wao wa sheria za Mungu, kuwaongoza kuja mbele ya madhabahu ya Mungu, kuwaongoza katika kuishi maisha miongoni mwa mambo mengine yote ambayo Mungu alikuwa amemuambia binadamu na yaliyomilikiwa na mpangilio na marudio ya mara kwa mara na ya kiasi. Kwanza Mungu alitumia taratibu na kanuni hizi rahisi kuweka vipimo kwa binadamu, ili hapa duniani binadamu aweze kuwa na maisha ya kawaida ya kumwabudu Mungu, aweze kuwa na maisha ya kawaida; hivi ndivyo yalivyo maudhui mahususi ya mwanzo wa mpango Wake wa usimamizi wa miaka elfu sita. Taratibu na sheria zinajumuisha maudhui mapana mno, yote ni maelezo ya mwongozo wa Mungu wa mwanadamu wakati wa

Enzi ya Sheria, lazima yangekubaliwa na kuheshimiwa na watu waliokuwa wamekuja kabla ya Enzi ya Sheria, ni rekodi ya kazi iliyofanywa na Mungu katika Enzi ya Sheria, na ni ithibati ya kweli ya uongozi na mwongozo wa Mungu kwa wanadamu wote.

Wanadamu Hawatenganishwi Milele na Mafundisho na Matoleo ya Mungu

Katika taratibu hizi tunaona kwamba mwelekeo wa Mungu katika kazi Yake, katika usimamizi Wake, na kwa wanadamu ukiwa wa kumakinikia zaidi, wa ukweli, wa bidii, na wa kuwajibika. Anaifanya kazi ambayo lazima Afanye miongoni mwa wanadamu kulingana na hatua Zake, bila ya hitilafu hata kidogo, Akiongea maneno ambayo lazima aongee kwa wanadamu bila ya kosa au upungufu hata kidogo, Akimruhusu binadamu kuona kwamba hawezi kutenganishwa na uongozi wa Mungu, na Akimwonyesha namna ambavyo yale yote ambayo Mungu anafanya na kusema yalivyo muhimu kwa wanadamu. Licha ya kile ambacho binadamu alivyo katika enzi ijayo, kwa ufupi, wakati wa mwanzo kabisa—wakati wa Enzi ya Sheria—Mungu alifanya mambo haya rahisi. Kwa Mungu, dhana za watu kumhusu Mungu, ulimwengu na mwanadamu katika enzi hiyo zilikuwa za kidhahania na zisizoeleweka, na ingawaje walikuwa na fikra na nia fulani husika, zote zilikuwa hazina uwazi na si sahihi, na hivyo wanadamu walikuwa hawawezi kutenganishwa kutoka kwa mafundisho na matoleo ya Mungu kwao. Wanadamu wa mapema zaidi hawakujua chochote, na hivyo Mungu alilazimika kuanza kumfunza binadamu kutoka kwenye kanuni za juujuu na za kimsingi zaidi kwa minajili ya uwepo na taratibu zinazohitajika za kuishi, kutia moyoni mambo haya yote kwenye moyo wa binadamu kidogo kidogo, na kumpa binadamu uelewa wa Mungu kwa utaratibu, kutambua na kuelewa uongozi wa Mungu kwa utaratibu, na dhana ya kimsingi ya uhusiano kati ya binadamu na Mungu, kupitia kwa taratibu hizi na kupitia kwa sheria hizi, ambazo zilikuwa za maneno. Baada ya kutimiza athari hii, ndipo tu Mungu aliweza, kidogo kidogo, kufanya kazi ambayo Angeweza kufanya baadaye, na hivyo taratibu hizi na kazi iliyofanywa na Mungu kwenye Enzi ya Sheria zikawa ndiyo msingi wa kazi Yake ya kuwaokoa wanadamu na hatua ya kwanza ya kazi katika mpango wa usimamizi wa Mungu. Ingawaje, kabla ya kazi ya Enzi ya Sheria, Mungu alikuwa ameongea naye Adamu, Hawa, na babu zao, amri na mafunzo hayo hayakuwa ya hatua kwa hatua sana au mahususi ili kutolewa moja baada ya nyingine kwa mwanadamu, na hayakuwa yameandikwa, wala hayakuwa taratibu. Hii ni kwa sababu, kwa wakati huo, mpango wa Mungu haukuwa umeenda mbali kiasi hicho; na Mungu alipokuwa amemwongoza binadamu hadi katika hatua hii tu ndipo Alipoweza kuongea taratibu hizi za Enzi ya Sheria, na kuanza kumfanya binadamu kuzitekeleza. Ulikuwa ni mchakato unaohitajika, na matokeo yasingeweza kuepukika. Tamaduni na taratibu hizi rahisi zinaonyesha binadamu hatua za usimamizi wa kazi ya Mungu na hekima ya Mungu inayofichuliwa katika mpango Wake wa usimamizi. Mungu anayajua maudhui yapi na mbinu zipi za kutumia ili kuanza, mbinu zipi za kutumia kuendelea na

mbinu zipi za kutumia kumaliza ili aweze kupata kundi la watu lililo na ushuhuda Kwake Yeye, Aweze kupata kundi la watu walio na akili sawa na Yake. Anajua kile kilicho ndani ya binadamu, na kujua kile kinachokosa kwa binadamu, Anajua kile anachofaa kutoa, na namna Anavyofaa kumwongoza binadamu, na pia ndivyo Anavyojua kile binadamu anafaa na hafai kufanya. Binadamu ni kama kikaragosi: Ingawaje hakuwa na uelewa wowote wa mapenzi ya Mungu, alilazimika kuongozwa na kazi ya Mungu ya usimamizi, hatua kwa hatua hadi leo. Hakukuwa na kutodhihirika kokote katika moyo wa Mungu kuhusu kile Alichofaa kufanya; katika moyo Wake kulikuwa na mpango wazi na kamilifu kabisa, na Alitekeleza kazi hiyo ambayo Yeye mwenyewe alitaka kufanya kulingana na hatua Zake na mpango Wake, Akiendelea mbele kutoka katika hali ya juujuu hadi ile hali ya ndani kabisa. Ingawaje Hakuwa ameonyesha kazi ambayo Alifaa kufanya baadaye, kazi Yake ya baadaye bado iliendelea kutekelezwa na kuendelea mbele kulingana kabisa na mpango Wake, ambayo ni maonyesho ya kile Mungu anacho na alichio, na pia ni mamlaka ya Mungu. Licha ya ni awamu gani ya mpango Wake wa usimamizi ambayo Anafanya, tabia Yake na kiini chake kinamwakilisha Yeye mwenyewe—na hakuna kosa katika haya. Licha ya enzi, au awamu ya kazi, aina ya watu ambao Mungu anapenda, aina ya watu ambao Anachukia, tabia Yake, na chote ambacho Anacho na alichio hakitawahi kubadilika. Ingawaje taratibu na kanuni hizi ambazo Mungu alianzisha katika kazi ya Enzi ya Sheria zinaonekana rahisi na za juujuu kwa watu wa leo, na Ingawaje ni rahisi kuelewa na kutimiza, ndani ya hizo kunayo bado hekima ya Mungu, na kunayo bado tabia ya Mungu na kile Anacho na alichio. Kwani ndani ya taratibu hizi zinazoonekana rahisi, uwajibikaji na utunzaji wa Mungu kwa wanadamu unaonyeshwa, na kiini kizuri cha fikira zake, kumruhusu binadamu kutambua kwa kweli ukweli kwamba Mungu anatawala mambo yote na mambo yote yanadhibitiwa kwa mkono Wake. Haijalishi ni kiwango kipi cha maarifa ambacho wanadamu watajifunza au nadhari au mafumbo mangapi wanaelewa, kwa Mungu hakuna chochote kati ya hivi ambavyo vinaweza kusawazisha toleo Lake kwa, na uongozi wa wanadamu; wanadamu milele hawatatenganishwa na mwongozo wa Mungu na kazi ya kibinafsi ya Mungu. Huu ndiyo uhusiano kati ya binadamu na Mungu usiotenganishwa. Licha ya kama Mungu anakupa amri, au taratibu, au Anakupa ukweli ili kuyaelewa mapenzi Yake, haijalishi ni nini Anachofanya, nia ya Mungu ni kumwongoza binadamu hadi katika siku nzuri ya kesho. Maneno yaliyotamkwa na Mungu na kazi Anayofanya ni ufunuo wa kipengele kimoja cha kiini Chake na vilevile ni ufunuo wa kipengele kimoja cha tabia Yake na hekima Yake, zote hizi ni hatua zisizozuilika katika mpango Wake wa usimamizi. Hili halifai kupuuzwa! Mapenzi ya Mungu yamo katika chochote Anachofanya; Mungu haogopi maoni yasiyo mahali pake wala haogopi dhana au fikira zozote za binadamu kuhusu Yeye. Yeye hufanya kazi Yake tu na kuendeleza usimamizi Wake kulingana na mpango Wake wa usimamizi, usiozuiliwa na mtu yeyote, suala lolote au kifaa chochote.

Vyema. Ni hayo tu kwa leo. Tuonane wakati mwingine!

Novemba 9, 2013

Kazi ya Mungu, Tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe III

Vikao hivi kadhaa vya ushirika vimekuwa na athari kubwa kwa kila mmoja wa watu. Kwa sasa, watu wanaweza hatimaye kuhisi uwepo wa kweli wa Mungu na kwamba Mungu kwa hakika yuko karibu sana na wao. Ingawa watu wamemwamini Mungu kwa miaka mingi, hawajawahi kuelewa kwa kweli mawazo na fikira Zake kama wanavyozielewa sasa, wala hawajawahi kupata kwa kweli uzoefu wa matendo Yake halisi kama walio nao kwa sasa. Kama ni maarifa au matendo halisi, watu wengi wamejifunza kitu kipya na kutimiza ufahamu wa juu zaidi, na wametambua kosa lililopo katika ufuatiliaji wao wa kale, wametambua hali yao waliyopitia ya juujuu na kwamba mambo mengi sana hayaambatani na mapenzi ya Mungu, na wametambua kwamba kile ambacho binadamu amepungukiwa nacho zaidi ni maarifa ya tabia ya Mungu. Maarifa haya kwa upande wa watu ni aina ya maarifa ya utambuzi; kufikia kiwango cha maarifa ya kirazini kunahitaji ushughulikiaji wa kina na utiliaji mkazo wa utaratibu kwenye hali yao yote wanayopitia. Kabla ya binadamu kumwelewa Mungu kwa njia ya kweli, kwa dhahania inaweza kusemekana kwamba wanaamini kwa uwepo wa Mungu mioyoni mwao, lakini hawana ufahamu halisi wa maswali mahususi kama vile Yeye ni Mungu wa aina gani kwa hakika, mapenzi Yake ni nini, tabia Yake ni ipi, na mtazamo Wake halisi kwa binadamu ni upi. Hali hii huhusisha pakubwa imani ya watu katika Mungu—imani yao haiwezi kwa ufupi kufikia utakatifu au ukamilifu. Hata kama utakuwa ana kwa ana na neno la Mungu, au kuhisi kwamba umekumbana na Mungu kupitia katika hali zako ulizopitia, bado haiwezi kusemwa kwamba unamwelewa Yeye kabisa. Kwa sababu hujui fikira za Mungu, au kile Anachopenda na kile Anachochukia, kile kinachomfanya kuwa na ghadhabu na kile kinachomletea furaha, huna ufahamu wa kweli kumhusu. Imani yako imejengwa katika msingi wa hali isiyokuwa dhahiri na ile ya fikira, kwa msingi wa matamania yako ya dhahania. Bado ingali mbali na imani halisi, na wewe bado ungali mbali na kuwa mfuasi wa kweli. Fafanuzi za mifano kutoka kwenye hadithi hizi za Biblia zimemruhusu binadamu kuujua moyo wa Mungu, kujua ni nini Yeye Alichokuwa akifikiria katika kila hatua ya kazi Yake na kwa nini Aliifanya kazi hii, nia Yake ya asili ilikuwa nini na mpango Wake ulikuwa upi Alipofanya kazi ile, namna ambavyo Alifikia fikira Zake na namna Alivyojitayarisha na kuendeleza mpango Wake. Kupitia katika hadithi hizi, tunaweza kupata ufahamu mahususi wenye maelezo ya kina, ya kila nia mahususi ya Mungu na kila wazo halisi wakati wa kazi Yake ya usimamizi ya miaka elfu sita, na mtazamo Wake kwa binadamu katika nyakati tofauti na enzi tofauti. Kuelewa kile ambacho Mungu alikuwa Anafikiria, mtazamo Wake ulikuwa upi na tabia Aliyoifichua alipokuwa Akikumbana na kila hali, kunaweza

kumsaidia kila mtu kwa kina zaidi kuweza kutambua kuwepo Kwake kwa hakika, na kuhisi kwa kina zaidi ukweli na uhalisi Wake. Lengo Langu katika kusimulia hadithi hizi si kwamba watu waweze kuelewa historia ya kibiblia, wala si kuwasaidia kupata uzoefu wa vitabu vya Biblia au watu walio ndani yake, na hasa si kuwasaidia watu kuelewa maelezo zaidi kuhusu kile ambacho Mungu alifanya katika Enzi ya Sheria. Ni kuwasaidia watu kuelewa mapenzi ya Mungu, tabia Yake, na kila sehemu ndogo Yake, na kuongeza ufahamu na maarifa ya Mungu yenye uhalisi zaidi na usahihi zaidi. Kwa njia hii, mioyo ya watu inaweza, hatua kwa hatua, kufunguka kwa ajili ya Mungu na kuwa karibu zaidi na Mungu, na wanaweza kumwelewa Yeye zaidi, tabia Yake, kiini Chake, na kumjua vema zaidi Mungu wa kweli Mwenyewe.

Ufahamu wa tabia ya Mungu na kile Alichio nacho na kile Alichio vinaweza kuwa na athari nzuri kwa binadamu. Vinaweza kuwasaidia kuwa na imani zaidi kwa Mungu, na kuwasaidia kufanikisha utiifu wa kweli na uchaji Kwake. Basi, wao tena si wafuasi wasioona, au wanaomwabudu tu bila mpango. Mungu hataki wajinga au wale wanaofuata umati bila mpango, lakini Anataka kundi la watu ambao wana ufahamu na maarifa wazi katika mioyo yao kuhusu tabia ya Mungu na wanaweza kuchukua nafasi ya mashahidi wa Mungu, watu ambao hawawezi kamwe kumwacha Mungu kwa sababu ya uzuri Wake, kwa sababu ya kile Alichio nacho na kile Alichio, na kwa sababu ya tabia Yake ya haki. Kama mfuasi wa Mungu, endapo katika moyo wako bado kuna ukosefu wa ubayana, au kuna hali tata au mkanganyo kuhusu kuwepo kwa kweli kwa Mungu, tabia Yake, kile Alichio nacho na kile Alichio, na mpango Wake wa kumwokoza binadamu, basi imani yako haiwezi kupata sifa za Mungu. Mungu hataki mtu wa aina hii kumfuata Yeye, na pia Hapendi mtu wa aina hii akija mbele Yake. Kwa sababu mtu wa aina hii hamwelewi Mungu, hawezi kutoa moyo wake kwa Mungu—moyo wake umemfungwa Kwake, hivyo basi imani yake katika Mungu imejaa kasoro mbalimbali. Kumfuata kwake Mungu kunaweza tu kusemwa kuwa ni kwa kipumbavu. Watu wanaweza tu kupata imani ya kweli na kuwa wafuasi wa kweli kama watakuwa na ufahamu na maarifa ya kweli wa Mungu, jambo ambalo linaleta utiifu na uchaji wa kweli Kwake. Ni kwa njia hii tu ndiyo anaweza kuutoa moyo wake kwa Mungu, kuufungua Kwake. Hili ndilo Mungu anataka, kwa sababu kila kitu wanachofanya na kufikiria, kinaweza kustahimili majaribu ya Mungu, na kinaweza kumshuhudia Mungu. Kila kitu Ninachowasiliana nanyi kuhusiana na tabia ya Mungu, au kuhusu kile Alichio nacho na kile Alichio, au mapenzi Yake na fikira Zake katika kila kitu Anachofanya, na kutoka kwenye mtazamo wowote ule, kutoka kwa upande wowote ule Nakizungumzia, yote haya ni kukusaidia kuwa na uhakika zaidi kuhusu uwepo wa kweli wa Mungu, na kuelewa na kushukuru zaidi kwa kweli upendo Wake kwa mwanadamu, na kuelewa na kufahamu vyema zaidi kwa kweli kile anachojali Mungu kuhusu binadamu, na tamania Lake la dhati la kumsimamia na kumwokoza mwanadamu.

Leo kwanza kabisa tutafanya muhtasari wa fikira, mawazo, na kila hatua ya Mungu tangu Alipomuumba binadamu, na kuangalia ni kazi gani Alitekeleza kuanzia uumbaji wa ulimwengu hadi mwanzo rasmi wa Enzi ya Neema. Tunaweza kisha kugundua ni fikira na mawazo yapi ya Mungu ambayo hayajulikani kwa binadamu, na kuanzia hapo tunaweza kuweka wazi mpangilio wa mpango wa usimamizi wa Mungu na kuelewa kwa kina muktadha ambao kwao Mungu alianzisha kazi Yake ya usimamizi, chanzo chake na mchakato wake wa maendeleo, na pia kuelewa kwa undani ni matokeo yapi Anayotaka kutoka katika kazi Yake ya usimamizi—yaani, kiini na kusudio la kazi Yake ya usimamizi. Kuelewa mambo haya tunahitaji kurudi hadi ule wakati wa kitambo, mtulivu na kimya ambapo hakukuwa na binadamu ...

Wakati Mungu aliinuka kutoka kitandani Mwake, fikira ya kwanza Aliyokuwa nayo ilikuwa hii: kumuumba binadamu hai, halisi, binadamu anayeishi—mtu wa kuishi naye na kuwa mwenzake wa kila mara. Mtu huyu angemsikiliza, na Mungu angempa siri Zake na kuongea na yeye. Kisha, kwa mara ya kwanza, Mungu aliuchukua udongo kwenye mkono na kuutumia kumuumba mtu wa kwanza kabisa aliye hai ambaye Alikuwa amemfikiria, na kisha Akakipa kiumbe hiki hai jina—Adamu. Punde Mungu alipompata mtu huyu aliye hai na anayepumua, Alihisi vipi? Kwa mara ya kwanza, Alihisi furaha ya kuwa na mpendwa, na mwandani. Aliweza kuhisi pia kwa mara ya kwanza uwajibikaji wa kuwa baba pamoja na kujali kunakoandamana na hisia hizo. Mtu huyu aliye hai na anayepumua alimletea Mungu furaha na shangwe; Alihisi aliyefarijika kwa mara ya kwanza. Hili lilikuwa jambo la kwanza ambalo Mungu aliwahi kufanya ambalo halikukamilishwa kwa fikira Zake au hata matamshi Yake, lakini lilifanywa kwa mikono Yake miwili. Wakati kiumbe aina hii—mtu aliye hai na anayepumua—aliposimama mbele ya Mungu, aliyeumbwa kwa nyama na damu, aliye na mwili na umbo, na aliyeweza kuongea na Mungu, Alihisi aina ya shangwe ambayo Hakuwa amewahi kuhisi kabla. Kwa kweli alihisi kwamba uwajibikaji Wake na kiumbe huyu hai haukuwa na uhusiano tu katika moyo Wake, lakini kila jambo dogo alilofanya pia lililingusa na likaupa moyo Wake furaha. Kwa hivyo wakati kiumbe huyu hai aliposimama mbele ya Mungu, ilikuwa ndiyo mara ya kwanza kuwahi kufikiria kuwapata watu wengi zaidi kama hawa. Huu ndio uliokuwa msururu wa matukio ulioanza kwa fikira hii ya kwanza ambayo Mungu alikuwa nayo. Kwa Mungu, matukio haya yote yalikuwa yakifanyika kwa mara ya kwanza, lakini katika matukio haya ya kwanza, haijalishi vile Alivyohisi wakati huo—furaha, uwajibikaji, kujali—hakukuwa na yeyote yule wa kushiriki furaha hii na Yeye. Kuanzia wakati huo, Mungu alihisi kwa kweli upweke na huzuni ambayo Hakuwahi kuwa nao mbeleni. Alihisi kwamba binadamu wasingekubali au kuelewa mapenzi Yake na kujali Kwake, au nia Zake kwa mwanadamu, hivyo basi Alihisi huzuni na maumivu katika moyo Wake. Ingawa Alikuwa amefanya mambo haya kwa binadamu, binadamu hakuwa na habari na hakuelewa. Mbali na furaha, shangwe na hali njema ambayo binadamu

alimletea pia viliandamana kwa haraka na hisia Zake za kwanza za huzuni na upweke. Hizi ndizo zilizokuwa fikira na hisia za Mungu wakati huo. Mungu alipokuwa akifanya mambo haya yote, moyoni Mwake Alitoka katika furaha Akaingia katika huzuni na kutoka katika huzuni Akaingia katika maumivu, vyote vikiwa vimechanganyika na wasiwasi. Kile Alichotaka kufanya tu kilikuwa kuharakisha kumruhusu mtu huyu, kizazi hiki cha binadamu kujua ni nini kilichokuwa moyoni Mwake na kuelewa nia Zake haraka iwezekanavyo. Kisha, wangukuwa wafuasi Wake na kupatana na Yeye. Wasingemsikiliza tena Mungu akiongea na kubakia kimya; wasingeendelea kutojua namna ya kujiunga na Mungu katika kazi Yake, na zaidi ya yote, wasingekuwa tena watu wasiojali na kuelewa mahitaji ya Mungu. Mambo haya ya kwanza ambayo Mungu alikamilisha ni yenye maana sana na yanashikilia thamani nyingi kwa minajili ya mpango Wake wa usimamizi na ule wa binadamu leo.

Baada ya kuviumba viumbe vyote na binadamu, Mungu hakupumzika. Asingesubiri kuutekeleza usimamizi Wake wala Asingeweza kusubiri kuwapata watu Aliowapenda mno miongoni mwa wanadamu.

Kisha, si kipindi kirefu baada ya Mungu kuwaumba binadamu, tunaona kutoka katika Biblia ya kwamba kulikuwa na gharika kubwa kote ulimwenguni. Nuhu anatajwa kwenye rekodi ya gharika, na inaweza kusemekana kwamba Nuhu ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kupokea mwito wa Mungu ili afanye kazi na Yeye ili kukamilisha kazi ya Mungu. Bila shaka, wakati huo ndio uliokuwa pia wa kwanza kwa Mungu kumwita mtu ulimwenguni kufanya kitu kulingana na amri Yake. Mara tu Nuhu alipokamilisha kuijenga safina, Mungu alileta gharika katika nchi kwa mara ya kwanza. Mungu alipoiharibu nchi kwa gharika, ndiyo ilikuwa mara ya kwanza tangu kuviumba viumbe ambapo Alihisi kuzidiwa na maudhi kwa binadamu; hili ndilo lililomlazimu Mungu kufanya uamuzi wa uchungu wa kuharibu kizazi hiki cha binadamu kupitia kwa gharika. Baada ya gharika kuiharibu dunia, Mungu alifanya agano Lake la kwanza na binadamu kwamba Hatawahi kufanya hivi tena. Ishara ya agano hili ilikuwa upinde wa mvua. Hili ndilo lililokuwa agano la kwanza la Mungu na binadamu, hivyo basi upinde wa mvua ndio uliokuwa ishara ya kwanza ya agano lililotolewa na Mungu; upinde huu wa mvua ni jambo halisi lililopo. Ni kule kuwepo kabisa kwa upinde huu wa mvua ambako humfanya Mungu mara nyingi ahisi huzuni kutokana na kizazi cha binadamu cha awali ambacho Amepoteza, na huwa ni kumbusho la kila mara Kwake kuhusiana na kile kilichowafanyikia.... Mungu asingepunguza mwendo Wake—Asingesubiri kuchukua hatua ya kufuata katika usimamizi Wake. Hivyo basi, Mungu alimchagua Ibrahimu kama chaguo Lake la kwanza kwa kazi Yake kote kote Israeli. Hii ndiyo iliyokuwa pia mara ya kwanza kwa Mungu kumchagua mteuliwa kama huyo. Mungu aliamua kuanza kutekeleza kazi Yake ya kumwokoza binadamu kupitia kwa mtu huyu, na kuendeleza kazi Yake miongoni mwa vizazi vya mtu huyu. Tunaweza kuona katika Biblia kwamba hivi ndivyo Mungu

alivyomfanyia Ibrahimu. Basi Mungu akaifanya Israeli kuwa nchi ya kwanza iliyochaguliwa, na Akaianza kazi Yake ya Enzi ya Sheria kupitia kwa watu Wake waliochaguliwa, Waisraeli. Tena kwa mara ya kwanza, Mungu aliwapa Waisraeli sheria na kanuni za moja kwa moja ambazo mwanadamu anafaa kufuata, na Akazieleza kwa kina. Hii ndiyo ilikuwa mara ya kwanza kwa Mungu kumpatia binadamu sheria kama hizo mahususi na wastani kuhusu namna wanavyofaa kutoa kafara, namna wanavyofaa kuishi, kile wanachofaa kufanya na kutofanya, ni sherehe na siku gani wanazofaa kutilia maanani, na kanuni za kufuata katika kila kitu walichofanya. Hii ndiyo iliyokuwa mara ya kwanza kwa Mungu kumpa binadamu taratibu na kanuni hizo zenye maelezo na uwastani kwa ajili ya maisha yao.

Ninaposema “mara ya kwanza,” inamaanisha Mungu hakuwa Amewahi kukamilisha kazi kama hiyo tena. Ni kitu ambacho hakikuwepo awali, na hata ingawa Mungu alikuwa Amemuumba binadamu na Alikuwa ameumba aina zote za viumbe na vitu vyenye uhai, Hakuwa amewahi kukamilisha kazi ya aina hiyo. Usimamizi wa Mungu kwa binadamu; yote ilihusu binadamu na wokovu Wake na usimamizi wa binadamu. Baada ya Ibrahimu, Mungu alifanya chaguo tena kwa mara ya kwanza—Alimchagua Ayubu kuwa ndiye chini ya sheria ndiye ambaye angestahimili majaribio ya Shetani huku akiendelea kumcha Mungu na kujiepusha na uovu na kuweza kumtolea Yeye ushuhuda. Hii pia ndiyo iliyokuwa mara ya kwanza kwa Mungu kuruhusu Shetani kumjaribu mtu na mara ya kwanza Alipoweka dau na Shetani. Mwishowe, kwa mara ya kwanza, Mungu alimpata mtu aliyekuwa na uwezo wa kusimama kama shahidi Wake huku akiwa amemkabili Shetani—mtu ambaye angeweza kumshuhudia Yeye na kumwaibisha kabisa Shetani. Tangu Mungu alipomuumba mwanadamu, huyu ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza, aliyempata ambaye aliweza kumshuhudia Yeye. Punde alipokuwa amempata mtu huyu, Mungu alikuwa na hata hamu zaidi ya kuendeleza usimamizi Wake na kuchukua hatua inayofuata katika kazi Yake, Akitayarisha chaguo Lake lifuatalo na mahali Pake pa kazi.

Baada ya kushiriki kuhusu haya yote, je, mnao ufahamu wa kweli wa mapenzi ya Mungu? Mungu anazingatia tukio hili la usimamizi Wake wa binadamu, la wokovu Wake wa binadamu, kama muhimu sana kuliko chochote kingine. Huyafanya mambo haya yote si kwa kutumia akili Zake tu, wala si kwa kutumia maneno Yake tu, na vilevile Yeye hafanyi hivi hususan kwa juujuu tu—Yeye huyafanya mambo haya yote kwa mpango, kwa viwango, na kwa mapenzi Yake. Ni wazi kwamba kazi hii ya kumwokoza binadamu imeshikilia umuhimu mkubwa kwa Mungu na hata binadamu. Haijalishi kazi ilivyo ngumu, haijalishi changamoto ni kubwa jinsi gani, haijalishi binadamu ni wanyonge jinsi gani, au binadamu amekuwa mwasi wa kweli, hakuna chochote kati ya haya ambacho ni kigumu kwa Mungu. Mungu hujibidiisha Mwenyewe, Akitumia jitihada Zake za bidii za kazi na kusimamia kazi ambayo Yeye Mwenyewe Anataka kutekeleza. Yeye pia Anapanga kila kitu na kuwatawala watu wote na kazi ambayo Anataka

kukamilisha—hakuna chochote kati ya haya ambacho kimefanywa awali. Ndiyo mara ya kwanza Mungu ametumia mbinu hizi na kulipa gharama kubwa kwa minajili ya mradi huu mkubwa wa kusimamia na kumwokoza mwanadamu. Huku Mungu akiwa Anatekeleza kazi hii, hatua kwa hatua Anawaonyesha na kuachilia kwa wanadamu bila kuficha juhudi Zake nyingi, kile Alichonacho na kile Alichokile, hekima na uweza, na kila dhana ya tabia Yake. Anaachilia na kuonyesha haya yote kwa mwanadamu kidogo kidogo, Akifichua na kuonyesha mambo haya kwa namna ambayo Hajawahi kufanya awali. Kwa hivyo, katika ulimwengu mzima, mbali na watu ambao Mungu analenga kuwasimamia na kuwaokoa, hakujawahi kuwepo na viumbe vyovyote vilivyo karibu na Mungu, ambavyo vinao uhusiano wa karibu sana na Yeye. Katika moyo Wake, yule mwanadamu Anayetaka kumsimamia na kumwokoza ndiye muhimu zaidi, na Anamthamini mwanadamu huyu zaidi ya kitu kingine chochote; hata ingawa Amelipia gharama ya juu na ingawa Anaumizwa na kutosikilizwa bila kukoma na wao, Hakati tamaa na Anaendelea bila kuchoka katika kazi Yake bila ya malalamiko au majuto. Hii ni kwa sababu Anajua kwamba hivi karibuni au baadaye, binadamu siku moja wataitikia mwito Wake na kuguswa na maneno Yake, kutambua kwamba Yeye ndiye Bwana wa uumbaji, na kurudi upande Wake ...

Baada ya kusikia haya yote leo, mnaweza kuhisi kwamba kila kitu ambacho Mungu anafanya ni kawaida sana. Yaonekana kwamba binadamu siku zote wamehisi mapenzi fulani ya Mungu kwao kutokana na matamshi Yake na pia kazi Yake, lakini siku zote kuna umbali fulani katikati ya hisia zao au maarifa yao na kile ambacho Mungu anafikiria. Kwa hivyo, Nafikiri ni muhimu kuwasiliana na watu wote kuhusu ni kwa nini Mungu alimuumba mwanadamu, na maelezo zaidi yanayoonyesha tamanio Lake la kuwapata watu aliokuwa Akitumainia. Ni muhimu kushiriki habari hii na kila mmoja, ili kila mmoja aweze kuwa wazi moyoni mwake. Kwa sababu kila fikira na wazo la Mungu, na kila awamu na kila kipindi cha kazi Yake vinafungamana ndani ya, na vyote hivi vimeunganishwa kwa karibu na, usimamizi Wake mzima wa kazi, unapoelewa fikira na mawazo ya Mungu, na mapenzi Yake katika kila hatua ya kazi Yake, ni sawa na ufahamu wa chanzo cha kazi ya mpango Wake wa usimamizi. Ni katika msingi huu ndipo ufahamu wako wa Mungu unapoanza kuwa wa kina. Ingawa kila kitu ambacho Mungu alifanya Alipoumba kwanza ulimwengu ambacho Nilitaja awali ni taarifa fulani tu kwa watu sasa na yaonekana kwamba hayana umuhimu sana katika utafutaji wa ukweli, katika mkondo wa kile ambacho utapitia kutakuwa na siku ambapo hutafikiria kuwa ni jambo rahisi sana kama mkusanyiko tu wa taarifa, wala kwamba ni kitu rahisi sana kama mafumbo fulani. Kwa kadri maisha yako yanavyoendelea na pale ambapo pana msimamo kidogo wa Mungu katika moyo wako, au unapokuja kuelewa waziwazi na kwa kina mapenzi Yake, utaweza kuelewa kwa kweli umuhimu na haja ya kile Ninachozungumzia leo. Haijalishi ni kwa kiwango kipi umeyakubali haya; ni muhimu kwamba uelewe na ujue mambo haya. Wakati Mungu

anapofanya jambo, wakati Anapotekeleza kazi Yake, haijalishi kama amefanya na mawazo Yake au kwa mikono Yake, haijalishi kama ni mara ya kwanza ambapo Amelifanya au kama ni mara ya mwisho—mwishowe, Mungu anao mpango, na makusudio Yake na fikira Zake vyote vimo katika kila kitu Anachokifanya. Makusudio na fikira hizi vinawakilisha tabia ya Mungu, na vinaonyesha kile Alichio nacho na kile Alichio. Vitu hivi viwili—tabia ya Mungu na kile Alichio nacho na kile Alichio—lazima vieleweke na kila mmoja. Punde mtu anapoelewa tabia Yake na kile Alichio nacho na kile Alichio, atanza kuelewa kwa utaratibu ni kwa nini Mungu anafanya kile Anachofanya na kwa nini Anasema kile Anachosema. Kutokana na hayo, anaweza kuwa na imani zaidi ya kumfuata Mungu, kuufuatilia ukweli, na kufuatilia mabadiliko katika tabia. Hivyo ni kusema, ufahamu wa binadamu kuhusu Mungu na imani yake katika Mungu haviwezi kutenganishwa.

Iwipo kile ambacho watu hupata ufahamu kuhusu au kupata kuelewa ni tabia ya Mungu na kile Alichio nacho na kile Alichio, basi kile wanachofaidi kitakuwa ni maisha yanayotoka kwa Mungu. Baada ya maisha haya kuhemshwa ndani yako, uchaji wako wa Mungu utakuwa mkubwa zaidi na zaidi, na kuvuna mavuno haya kunafanyika kwa kawaida sana. Kama hutaki kuelewa au kujua kuhusu tabia ya Mungu au kiini Chake, kama hutaki hata kutafakari juu ya mambo haya au kuyazingatia, Naweza kukuambia kwa hakika kwamba hiyo njia unayoifuatilia katika imani yako kwa Mungu haitawahi kukuruhusu kuyaridhisha mapenzi Yake au kupata sifa Zake. Zaidi ya hayo, huwezi kamwe kufikia wokovu—hizi ndizo athari za mwisho. Wakati watu hawamwelewi Mungu na hawajui tabia Yake, mioyo yao haiwezi kamwe kuwa wazi Kwake. Punde wanapomwelewa Mungu, wataanza kuthamini na kufurahia kile kilicho moyoni Mwake kwa kivutio na imani. Unapothamini na kufurahia kile kilichomo ndani ya moyo wa Mungu, moyo wako utanza kwa utaratibu, kidogokidogo, kuwa wazi Kwake. Wakati moyo wako unakuwa wazi Kwake, utahisi namna ambavyo mabadilishano yako na Mungu yataavyokuwa ya aibu na duni, madai yako kutoka kwa Mungu na matamanio yako mengi binafsi. Moyo wako unapofunguka kwa kweli kwa Mungu, utaona kwamba moyo Wake ni ulimwengu usio na mwisho, na utaingia katika ulimwengu ambao hujawahi kuupitia awali. Katika ulimwengu huu hakuna kudanganya, hakuna udanganyifu, hakuna giza, hakuna maovu. Kunao ukweli wa dhati na uaminifu; kunayo nuru na uadilifu tu; kunayo haki na huruma. Umejaa upendo na utunzaji, umejaa rehema na uvumilivu, na kupitia katika ulimwengu huu utahisi shangwe na furaha ya kuwa hai. Mambo haya ndiyo ambayo Atakufichulia utakapoufungua moyo wako kwa Mungu. Hii dunia isiyo na kikomo imejaa hekima ya Mungu, na imejaa kudura Yake; umejaa pia upendo Wake na mamlaka Yake. Hapa unaweza kuona kila kipengele cha kile Mungu Alichio nacho na kile Alichio, ni nini kinachomletea Yeye shangwe, kwa nini Anakuwa na wasiwasi na kwa nini Anakuwa na huzuni, kwa nini Anakuwa na hasira.... Haya ndiyo ambayo kila mmoja

anayeufungua moyo wake na kumruhusu Mungu kuingia ndani anaweza kuona. Mungu anaweza tu kuingia katika moyo wako kama utaufungua kwa ajili Yake. Unaweza kuona tu kile Mungu Alichonacho na kile Alichonacho, na unaweza kuona tu mapenzi Yake kwako, kama Ameingia katika moyo wako. Wakati huo, utagundua kwamba kila kitu kuhusu Mungu ni chenye thamani, kwamba kile Alichonacho na kile Alichonacho kina thamani sana ya kuthaminiwa. Ukilinganisha na hayo, watu wanaokuzunguka, vifaa na matukio katika maisha yako, hata wapendwa wako, mwandani wako, na mambo unayopenda, si muhimu sana. Ni madogo mno, na ni ya kiwango cha chini; utahisi kwamba hakuna chombo chochote cha anasa ambacho kitaweza kukuvutia tena, na au kwamba kitu chochote yakinifu kitawahi kukushawishi tena ukilipie gharama yoyote tena. Kwa unyenyekevu wa Mungu utaona ukubwa Wake na mamlaka Yake ya juu; aidha, katika jambo Alilofanya uliloliamini kuwa dogo mno, utaweza kuona hekima Yake na uvumilivu Wake usio na mwisho, na utaiona subira Yake, uvumilivu Wake na ufahamu Wake kwako. Hili litazaa ndani yako upendo Kwake. Siku hiyo, utahisi kwamba mwanadamu anaishi katika ulimwengu mchafu, kwamba watu walio upande wako na mambo yanayokufanyikia katika maisha yako, na hata kwa wale unaopenda, upendo wao kwako, na ulinzi wao kama ulivyojulikana au kujali kwao kwako havistahili hata kutajwa—Mungu tu ndiye mpendwa wako na ni Mungu tu unayethamini zaidi. Wakati siku hiyo itawadia, Naamini kwamba kutakuwa na baadhi ya watu watakaosema: Upendo wa Mungu ni mkubwa na kiini Chake ni kitakatifu mno—ndani ya Mungu hakuna udanganyifu, hakuna uovu, hakuna wivu, na hakuna mabishano, lakini ni haki tu na uhalisi, na kila kitu Alichonacho Mungu na kile Alichonacho vyote vinafaa kutamaniwa na binadamu. Binadamu wanafaa kujitahidi na kuwa na hamu ya kuvipata. Ni kwa msingi gani ndipo uwezo wa mwanadamu wa kutimiza haya umejengwa? Unajengwa kwa msingi wa ufahamu wa binadamu wa tabia ya Mungu, na ufahamu wao kuhusu kiini cha Mungu. Hivyo basi kuelewa tabia ya Mungu na kile Alichonacho na kile Alichonacho, ni funzo la maisha yote kwa kila mtu na ni lengo la maisha yote linalofuatiliwa na kila mtu anayelenga kubadilisha tabia yake, na kutamani kumjua Mungu.

Tumezungumza tu kuhusu kazi yote ambayo Mungu amekamilisha, misururu ya mambo Aliyoyafanya kwa mara ya kwanza. Kila mojawapo ya mambo haya yanahusiana na mpango wa Mungu wa usimamizi na mapenzi ya Mungu. Yanahusiana pia na tabia binafsi ya Mungu na kiini Chake. Kama tunataka kuelewa zaidi ya kile Alichonacho Mungu na kile Alichonacho, sisi hatuwezi kukoma katika Agano la Kale au katika Enzi ya Sheria, lakini tunahitaji kusonga mbele pamoja na hatua ambazo Mungu alichukua katika kazi Yake. Hivyo basi, Mungu alipotamatisha Enzi ya Sheria na kuanza Enzi ya Neema, hatua zetu binafsi zimefika katika Enzi ya Neema—enzi iliyojaa neema na ukombozi. Katika enzi hii, Mungu tena Alifanya kitu cha muhimu sana kwa mara ya kwanza. Kazi katika enzi hii mpya kwa Mungu na hata kwa mwanadamu ilikuwa

sehemu mpya ya kuanzia. Sehemu hii mpya ya kuanzia ilikuwa tena kazi mpya ambayo Mungu alifanya kwa mara ya kwanza. Kazi hii mpya ilikuwa kitu ambacho hakikuwahi kutokea awali ambacho Mungu alitekeleza na hakikufikirika na binadamu na viumbe vyote. Ni kitu ambacho kwa sasa kinajulikana kwa watu wote—hii ndiyo iliyokuwa mara ya kwanza Mungu aligeuka kuwa binadamu, mara ya kwanza Alianza kazi mpya kwa umbo la binadamu, Akiwa na utambulisho wa mwanamume. Kazi hii mpya ilionyesha kwamba Mungu alikuwa Amekamilisha kazi Yake katika Enzi ya Sheria, kwamba Asingefanya au kusema tena chochote chini ya sheria. Wala Asingewahi tena kuzungumza au kufanya chochote kwa mfano wa sheria au kulingana na kanuni au masharti ya sheria. Yaani, kazi Yake yote inayotokana na sheria ilisitishwa milele na isingendelezwa, kwa sababu Mungu alitaka kuanza kazi mpya na kufanya mambo mapya, na mpango Wake kwa mara nyingine tena ulikuwa na sehemu mpya ya kuanzia. Hivyo basi, Mungu lazima Angemwongoza binadamu hadi katika enzi inayofuata.

Kama hii ilikuwa habari ya shangwe au ya kisirani kwa binadamu ilitegemea kiini chao kilikuwa kipi. Inaweza kusemekana kwamba hizi hazikuwa habari za shangwe, lakini zilikuwa habari za kisirani kwa baadhi ya watu, kwa sababu Mungu alipoanza kazi Yake mpya, watu hao ambao walifuata tu sheria na masharti, ambao walifuata tu kanuni lakini hawakumcha Mungu wangegemea upande wa kutumia kazi nzee ya Mungu ili kuishutumu kazi Yake mpya. Kwa watu hawa, hizi zilikuwa habari za kisirani; lakini kwa kila mtu aliyekuwa hana hatia na aliyekuwa wazi, aliyekuwa mwenye ukweli kwa Mungu na aliyekuwa radhi kupokea ukombozi Wake, Mungu kuwa mwili kwa mara ya kwanza zilikuwa habari zenye shangwe sana. Kwani tangu kuwepo na binadamu, hii ndiyo iliyokuwa mara ya kwanza Mungu kuonekana na kuishi miongoni mwa wanadamu katika umbo ambalo halikuwa Roho; badala yake, Alizaliwa na mwanadamu na kuishi miongoni mwa watu kama Mwana wa Adamu, na kufanya kazi katikati yao. Hii “mara ya kwanza” ilizivunja dhana za watu na pia ilikuwa zaidi ya kufikiria kote. Aidha, wafuasi wote wa Mungu walipata manufaa ya kushikika na kuonekana. Mungu hakuikomesha tu enzi nzee, lakini pia Alikomesha mbinu Zake za kale za kufanya kazi pamoja na mitindo ya kufanya kazi. Hakuruhusu tena wajumbe Wake kuwasilisha mapenzi Yake, na hakufichika tena katika mawingu na hakuonekana tena au kuongea kwa binadamu kupitia kwa ishara za amri kwa radi. Tofauti na chochote kile cha awali, kupitia kwa mbinu ambayo haikufirika kwa binadamu ambayo pia ilikuwa ngumu kwa wao kuelewa na kukubali—kupata mwili—Aligeuka na kuwa Mwana wa Adamu ili kuendeleza kazi ya enzi hiyo. Kitendo hiki cha Mungu kiliwashtua wanadamu; kiliwafanya wawe na aibu, kwa sababu Mungu kwa mara nyingine alikuwa ameanza kazi mpya ambayo Hakuwahi kufanya tena. Leo, tutaangalia ni kazi gani mpya ambayo Mungu alikamilisha katika enzi mpya, na katika haya yote ya kazi mpya, tabia ya Mungu nayo ilikuwa vipi, na nini Alichu nacho na kile Alichu ambayo tunaweza

kuelewa?

Yafuatayo ni maneno yaliyorekodiwa katika Agano Jipya la Biblia:

1. Mat 12:1 Wakati huo katika siku ya Sabato Yesu alipitia mashamba ya nafaka; na wanafunzi wake walihisi njaa, nao wakaanza kung’oa masuke ya nafaka na kuyala.

2. Mat 12:6-8 Lakini nasema kwenu, Kwamba mahali humu yumo aliye mkubwa kuliliko hekalu. Lakini iwapo mngejua maana ya hili, Naitaka rehema, na siyo sadaka, msingewashutumu wale wasio na hatia. Kwa sababu Mwana wa Adamu ni Bwana hata wa siku ya Sabato.

Hebu kwanza tuangalie dondoo hii: “Wakati huo katika siku ya Sabato Yesu alipitia mashamba ya nafaka; na wanafunzi wake walihisi njaa, nao wakaanza kung’oa masuke ya nafaka na kuyala.”

Kwa nini Nimeichagua dondoo hii? Dondoo hii ina uhusiano upi na tabia ya Mungu? Katika maandiko haya kitu cha kwanza tunachojua ni kwamba ilikuwa ni siku ya Sabato, lakini Bwana Yesu alipita kule nje na kuwaongoza wanafunzi Wake katika mashamba ya nafaka. Lakini kilicho telezi zaidi” ni kwamba waliweza hata “wakaanza kung’oa masuke ya nafaka na kuyala.” Katika Enzi ya Sheria, sheria za Yehova Mungu ilisema kwamba watu wasingeweza kuenda vivi hivi tu au kushiriki katika shughuli katika siku ya Sabato—kulikuwa na mambo mengi ambayo hayangefanywa siku ya Sabato. Hatua hii ya Bwana Yesu ilikuwa ya kuchanganya hasa kwa wale waliokuwa wameishi chini ya sheria kwa muda mrefu, na iliweza hata kuchochea upinzani mkubwa. Kuhusiana na mchanganyiko wao na namna walivyouzungumzia kile ambacho Yesu alifanya, tutaweka hilo pembeni kwa sasa na kuzungumzia kwanza kwa nini Bwana Yesu alichagua kufanya hivi katika siku ya Sabato, kwa siku zote, na kile Alichotaka kuwasilisha kwa watu waliokuwa wakiishi katika enzi ya kale kupitia katika hatua hii. Huu ndio uhusiano kati ya dondoo hii na tabia ya Mungu ambayo Ningependa kuzungumzia.

Bwana Yesu alipokuja, Alitumia vitendo Vyake vya utendaji kuwambia watu: kwamba Mungu alikuwa ameiondoa Enzi ya Sheria na alikuwa ameanza kazi mpya, na kwamba kazi hii mpya haikuhitaji utilifu maanani wa Sabato. Wakati Mungu kutoka katika mipaka ya siku ya Sabato, hicho kilikuwa tu kionjo cha mapema cha kazi Yake mpya. Bwana Yesu alipoanza kazi Yake, tayari Alikuwa ameacha nyuma zile pingu za Enzi ya Sheria, na alikuwa ametupilia mbali zile taratibu na kanuni zilizokuwa za enzi hiyo. Ndani yake hakuwa na dalili za chochote kuhusiana na sheria; Alikuwa ameitupa nje mzima mzima na hakuifuata tena, na Hakuhitaji tena mwanadamu kuifuata. Kwa hivyo hapa unaona kwamba Bwana Yesu alipita katika mashamba siku ya Sabato; Bwana hakupumzika lakini, alikuwa akipita kule nje akifanya kazi. Hatua hii Yake ilikuwa ya kushtua kwa dhana za watu na iliweza kuwawasilishia ujumbe kwamba

Hakuishi tena chini ya sheria na kwamba Alikuwa ameacha ile mipaka ya Sabato na kujitokeza mbele ya mwanadamu na katikati yao katika taswira mpya, huku akiwa na njia mpya ya kufanya kazi. Hatua hii Yake iliwaambia watu kwamba Alikuwa amelea pamoja naye kazi mpya iliyoanza kwa kwenda nje ya sheria na kwenda nje ya Sabato. Wakati Mungu alitekeleza kazi Yake mpya, Hakushikilia tena ya kale, na Hakujali tena kuhusu taratibu za Enzi ya Sheria. Wala Hakuathirika na kazi Yake mwenyewe katika enzi ya awali, lakini Alifanya kazi kwa kawaida katika siku ya Sabato na wakati wanafunzi Wake waliona njaa, waliweza kuvunja masuke na wakala. Haya yote yalikuwa kawaida sana machoni mwa Mungu. Mungu angeweza kuwa na mwanzo mpya kwa nyingi za kazi Anazotaka kufanya na mambo Anayotaka kusema. Punde Anapokuwa na mwanzo mpya, Hataji kazi Yake ya awali tena wala kuiendeleza. Kwani Mungu anazo kanuni Zake katika kazi Yake. Anapotaka kuanzisha kazi mpya, ndipo Anapotaka kumleta mwanadamu katika awamu mpya ya kazi Yake, na wakati kazi Yake imeingia katika awamu ya juu zaidi. Kama watu wanaendelea kutenda kulingana na misemo au taratibu za kale au kuendelea kushikilia kabisa kwazo, Hatakumbuka au kulisifu jambo hili. Hii ni kwa sababu tayari Ameileta kazi mpya, na ameingia katika awamu mpya ya kazi Yake. Anapoanzisha kazi mpya, Anaonekana kwa mwanadamu akiwa na taswira mpya kabisa, kutoka katika mtazamo mpya kabisa, na kwa njia mpya kabisa ili watu waweze kuona dhana zile tofauti za tabia Yake na kile Alichonacho na kile Alichonacho. Hii ni mojawapo ya malengo Yake katika kazi Yake mpya. Mungu hashikilii ya kale au kutumia njia isiyotumika na wengi; Anapofanya kazi na kuongea sio njia ya kutilia mipaka kama vile watu wanavyofikiria. Ndani ya Mungu, vyote ni huru na vimekombolewa, na hakuna hali ya kukinga, hakuna viziwi—kile Anachomletea mwanadamu vyote ni uhuru na ukombozi. Yeye ni Mungu aliye hai, Mungu ambaye kwa kweli, na kwa hakika yupo. Yeye si kikapotea au sanamu ya udongo, na Yeye ni tofauti kabisa na sanamu ambazo watu huhifadhi na kuabudu. Yeye yuko hai na mwenye nguvu na kile ambacho maneno Yake na kazi Yake humletea binadamu vyote ni uzima na nuru, uhuru na ukombozi wote, kwa sababu Yeye anashikilia ukweli, uzima, na njia—Yeye hajazuliwa na chochote katika kazi yoyote Yake. Bila kujali watu wanavyosema na namna wanavyoona au kukadiria kazi Yake mpya, Ataitekeleza kazi Yake bila hofu. Hatakuwa na wasiwasi kuhusu dhana zozote za yeyote au kazi na maneno Yake kuelekezewa vidole, au hata upinzani wao mkubwa katika kazi Yake mpya. Hakuna yeyote miongoni mwa viumbe vyote anayeweza kutumia akili ya binadamu, au kufikiria kwa binadamu, maarifa au maadili ya binadamu kupima au kufasili kile ambacho Mungu anafanya, kutia fedheha, au kutatiza au kukwamiza kazi Yake. Hakuna kizuizi chochote katika kazi Yake na kile Anachokifanya; na haitawekewa kizuizi chochote na binadamu yeyote, tukio, au kitu, wala haitakatizwa na nguvu zozote za kikatili. Kwa mjibu wa kazi Yake mpya kuhusika, Yeye ni Mfalme anayeshinda daima, na nguvu zozote za kikatili na uzushi wote na hoja za uwongo za mwanadamu zimekanyagiwa chini ya kibao Chake cha kuwekea miguu.

Haijalishi ni hatua gani mpya ya kazi Yake ambayo Anatekeleza, ni hakika itaendelezwa na ipanuliwe katika mwanadamu, na hakika itatekelezwa bila kuzuiliwa duniani kote mpaka pale ambapo kazi Yake kubwa imekamilika. Huu ndio uweza na hekima ya Mungu, na mamlaka na nguvu Zake. Hivyo basi, Bwana Yesu angeweza kwenda kule nje waziwazi na kufanya kazi katika siku ya Sabato kwa sababu ndani ya moyo Wake hakukuwa na sheria zozote, na hakukuwa na maarifa au kanuni zozote zilizotokana na binadamu. Kile Alichokuwa nacho kilikuwa ni kazi mpya ya Mungu na njia Yake, na kazi Yake ndio iliyokuwa njia ya kumweka huru mwanadamu, kumwachilia, kumruhusu kuwepo katika nuru na kumruhusu kuishi. Na wale wanaoabudu sanamu au miungu ya uwongo wanaishi kila siku wakiwa wamefungwa na Shetani, wakiwa wamezuiliwa na aina zote za sheria na mila—leo kitu kimoja hakiruhusiwi, kesho kingine—hakuna uhuru katika maisha yao. Wao ni sawa na wafungwa katika pingu wasio na shangwe ya kuzungumzia. “Kuzuiliwa” linawakilisha nini? Linawakilisha shurutisho, utumwa na uovu. Punde tu mtu anapoabudu sanamu, anaabudu mungu wa uwongo, akimwabudu roho wa uovu. Kuzuiliwa kunaenda sambamba na hilo. Huwezi kula hiki au kile, leo huwezi kwenda nje, kesho huwezi kuwasha jiko lako, siku inayofuata huwezi kuhamia katika nyumba mpya, siku fulani lazima zichaguliwe kwa minajili ya harusi na mazishi, na hata za wakati wa kujifungua mtoto. Haya yote yanaitwa nini? Haya yanaitwa kuzuiliwa; ni utumwa wa mwanadamu, na ndizo pingu za maisha za Shetani na roho wa maovu wanaowadhibiti, na wanaozuilia mioyo yao na mili yao. Je, kuzuiliwa huku kunapatikana kwa Mungu? Tunapozungumzia utakatifu wa Mungu, unafaa kwanza kufikiria haya: Kwa Mungu hakuna vizuizi. Mungu anazo kanuni katika maneno na kazi Yake, lakini hakuna kuzuiliwa, kwa sababu Mungu Mwenyewe ndiye ukweli, njia na uzima.

Sasa hebu tuangalie dondoo ifuatayo: “Lakini nasema kwenu, Kwamba mahali humu yumo aliye mkubwa kuliliko hekalu. Lakini iwapo mngejua maana ya hili, Naitaka rehema, na siyo sadaka, msingewashutumu wale wasio na hatia. Kwa sababu Mwana wa Adamu ni Bwana hata wa siku ya sabato” (Mat 12:6-8). “Hekalu” hapa linamaanisha nini? Kwa ufupi, “hekalu” linaashiria jengo refu la kupendeza, na katika Enzi ya Sheria, hekalu lilikuwa ni pahali pa makuhani kumwabudu Mungu. Bwana Yesu aliposema “mahali humu yumo aliye mkubwa kuliliko hekalu,” “mmoja” ilikuwa ikirejelea nani? Ni wazi, “mmoja” ni Bwana Yesu katika mwili kwa sababu Yeye tu ndiye aliyekuwa mkuu kuliko hekalu. Na maneno hayo yaliwaambia watu nini? Yaliwaambia watu watoke hekaluni—Mungu alikuwa tayari ameshatoka nje na hakuwa tena akifanyia kazi ndani yake, hivyo basi watu wanafaa kutafuta nyayo za Mungu nje ya hekalu na kufuata nyayo Zake katika kazi Yake mpya. Usuli wa Bwana Yesu kusema haya ilikuwa kwamba chini ya sheria, watu walikuwa wameiona hekalu kama kitu kilichokuwa kikuu zaidi kuliko Mungu Mwenyewe. Yaani, watu waliliabudu hekalu badala ya kumwabudu Mungu,

hivyo basi Bwana Yesu akawaonya kutoabudu sanamu, lakini kumwabudu Mungu kwa sababu Yeye ndiye mwenye mamlaka ya juu zaidi. Hivyo basi, alisema: “Naitaka rehema, na siyo sadaka.” Ni wazi kwamba katika macho ya Bwana Yesu, watu wengi sana katika sheria hawakumwabudu tena Yehova, lakini walikuwa tu wakipitia mchakato wa kutoa sadaka na Bwana Yesu aliamua kwamba mchakato huu ulikuwa ibada ya sanamu. Waabudu sanamu hawa waliliona hekalu kama kitu kikuu, cha juu zaidi kuliko Mungu. Ndani ya mioyo yao kulikuwa tu na hekalu, wala si Mungu, na kama wangelipoteza hekalu, wangepoteza mahali pao pa kukaa. Bila ya hekalu hawakuwa na mahali popote pa kuabudu na wasingeweza kutoa sadaka zao. Mahali pao pa kukaa kama palivyojulikana ndipo walipofanyia shughuli zao kwa jina la kumwabudu Yehova Mungu, na hivyo basi wakaruhusiwa kuishi katika hekalu na kutekeleza shughuli zao binafsi. Ule utoaji sadaka wao kama ulivyojulikana ulikuwa tu kutekeleza shughuli zao za kibinafsi za aibu wakisingizia kwamba walikuwa wanaendesha ibada yao katika hekalu. Hii ndiyo iliyokuwa sababu iliyowafanya watu wakati huo kuliona hekalu kuwa kuu kuliko Mungu. Kwa sababu walilitumia hekalu kama maficho, na sadaka kama kisingizio cha kuwadanganya watu na kumdanganya Mungu, Bwana Yesu alisema haya ili kuwaonya watu. Mkitumia maneno haya kwa wakati wa sasa, yangali bado halali na yenye umuhimu sawa. Ingawa watu wa leo wameweza kupitia kazi tofauti za Mungu kuliko watu wa Enzi ya Sheria walivyowahi kupitia, kiini cha asili yao ni kile kile. Katika muktadha wa kazi leo, watu bado watafanya aina sawa ya mambo kama yale ya “hekalu kuwa kuu kuliko Mungu”. Kwa mfano, watu huona kutimiza wajibu wao kama kazi yao; wanaona kutoa ushuhuda kwa Mungu na kupigana na joka kubwa jekundu kama harakati ya kisiasa ya kulinda haki za kibinadamu, kwa ajili ya demokrasia na uhuru; wao hugeuza wajibu wao ili kutumia weledi wao kuwa ajira, lakini wanachukulia kumcha Mungu na kujiepusha na maovu tu kama kipande cha kanuni ya kidini ya kufuatwa; na kadhalika. Je, maonyesho haya kwa upande wa binadamu hasa hayako sawa na “hekalu ni kuu kumlika Mungu”? Isipokuwa tu kwamba miaka elfu mbili iliyopita, watu walikuwa wakiendeleza shughuli zao za kibinafsi katika hekalu linaloshikika, lakini leo, watu wanaendeleza shughuli zao za kibinafsi katika mahekalu yasiyogusika. Wale watu wanaothamini masharti huona masharti kuwa kuu zaidi kuliko Mungu, wale watu wanaopenda hadhi huona hadhi kuu zaidi kuliko Mungu, wale watu wanaopenda ajira zao huziona ajira hizo kuwa kuu zaidi kuliko Mungu na kadhalika—maonyesho yao yote yananifanya Mimi kusema: “Watu humsifu Mungu kuwa ndiye mkuu zaidi kupitia kwa maneno yao, lakini kwa macho yao kila kitu ni kikuu zaidi kuliko Mungu.” Hii ni kwa sababu punde tu watu wanapopata fursa katika njia yao ya kumfuata Mungu ili kuonyesha vipaji vyao, au kuendelea na shughuli zao binafsi za kibiashara au ajira yao binafsi, wanakuwa mbali na Mungu na kufanya kwa bidii ajira wanayoipenda. Kuhusiana na kile ambacho Mungu amewaaminia, na mapenzi Yake, mambo hayo yote yametupiliwa mbali kitambo. Katika hali hii, ni nini tofauti baina ya watu hawa na

wale wanaoendesha biashara zao katika hekalu miaka elfu mbili iliyopita?

Kisha, hebu tuangalie sentensi ya mwisho katika dondoo hii ya maandiko: “Kwa sababu Mwana wa Adamu ni Bwana hata wa siku ya Sabato.” Je, kuna upande wa utendaji kwa sentensi hii? Je, unaweza kuona upande wa utendaji kwa sentensi hii? Kila kitu anachosema Mungu kinatoka moyoni Mwake, kwa hivyo kwa nini Alisema hivi? Unaelewa vipi sentensi hii? Unaweza kuelewa maana ya sentensi hii sasa, lakini wakati huo si watu wengi walikuwa wanaelewa kwa sababu binadamu alikuwa tu ametoka katika Enzi ya Sheria. Kwao, kutoka katika Sabato lilikuwa jambo gumu sana kufanya, sembuse kuelewa Sabato ya kweli ilikuwa nini.

Sentensi “Mwana wa Adamu ni Bwana hata wa siku ya Sabato.” inawaambia watu kwamba kila kitu cha Mungu ni visivyo vya mwili, na ingawa Mungu anaweza kukupa mahitaji yako yote ya kimwili, punde tu mahitaji yako yote ya mwili yametimizwa, utoshelevu unaotokana na mambo haya unaweza kuchukua nafasi ya ufuatiliaji wako wa ukweli? Kwa kweli hiyo haiwezekani! Tabia ya Mungu na kile Alichio nacho na kile Alichio ambayo tumeweza kushiriki pamoja ni kweli. Haiwezi kupimwa kupitia kwa gharama ya juu ya vifaa vya kimwili wala thamani yake kupimwa kwa pesa, kwa sababu si kifaa cha anasa, na kinatoa mahitaji ya moyo wa kila mmoja. Kwa kila mmoja, thamani ya ukweli huu usioshikika inafaa kuwa kubwa zaidi kuliko thamani ya vitu vyovyote vya anasa unavyofikiria kuwa ni vizuri, sivyo? Kauli hii ni kitu mnachohitaji kukiwazia. Hoja kuu ya kile nilichosema ni kwamba kile Alichio nacho Mungu na kile Alichio na kila kitu cha Mungu ndivyo vitu muhimu zaidi kwa kila mtu na haviwezi kubadilishwa na kifaa chochote cha anasa. Nitakupa mfano: Ukiwa na njaa, unahitaji chakula. Chakula hiki kinaweza kuwa kizuri kwa kiasi fulani au kinaweza kuwa kimekosa kitu fulani kwa kiasi fulani, lakini mradi tu umekula ukashiba, hisia ile mbaya ya kuwa na njaa haitakuwepo tena—itakuwa imeondoka. Unaweza kuketi pale kwa amani, na mwili wako utakuwa umepumzika. Njaa ya watu inaweza kutatuliwa kwa chakula, lakini ukiwa unamfuata Mungu na kuhisi kwamba huna ufahamu wowote Wake, unawezaje kutatua utupu huu katika moyo wako? Hali hii inaweza kusuluhishwa kwa chakula? Au unapomfuata Mungu na huelewi mapenzi Yake, ni nini unachoweza kutumia ili kufidia ile njaa katika moyo wako? Katika mchakato wa uzoefu wako wa wokovu kupitia kwa Mungu, wakati ukifuatilia mabadiliko katika tabia yako, kama huelewi mapenzi Yake au hujui ukweli ni nini, kama huelewi tabia ya Mungu, huhisi wasiwasi sana? Huhisi njaa na kiu kuu katika moyo wako? Je, hizi hisia hazikuzui dhidi ya kuhisi pumziko katika moyo wako? Hivyo basi unaweza kufidia vipi njaa hiyo katika moyo wako—kunayo njia ya kutatua suala hilo? Baadhi ya watu huenda kufanya ununuzi, baadhi hupata rafiki wa kuwaambia yaliyo moyoni, baadhi hulala mpaka watosheke, wengine husoma zaidi maneno ya Mungu, au wakatia bidii zaidi na kutumia jitihada nyingi zaidi kukamilisha wajibu wao. Je,

mambo haya yanaweza kutatua ugumu wako halisi? Nyinyi nyote mnaelewa kikamilifu aina hizi za mazoea. Unapohisi kuwa huna nguvu, unapohisi tamanio kubwa la kupata nuru kutoka kwa Mungu ili kukuruhusu kujua uhalisi wa ukweli na mapenzi Yake, ni nini unachohitaji kingi zaidi? Kile unachohitaji si mlo kamili, na wala si maneno machache mema. Zaidi ya hayo, si lile tulizo na kutosheka kwa muda kwa mwili—kile unachohitaji ni Mungu kuweza kukueleza moja kwa moja, kwa wazi kile unachofaa kufanya na namna unavyofaa kukifanya, kuweza kukuonyesha wazi ukweli ni nini. Baada ya kuelewa haya, hata kama ni sehemu ndogo tu, huhisi kuwa umetosheka zaidi katika moyo wako kuliko vile ambavyo ungekuwa umekula mlo mzuri? Wakati moyo wako umetosheka, huo moyo wako, nafsi yako nzima, havipati pumziko la kweli? Kutokana na mfano huu na uchambuzi, je, mnaelewa sasa ni kwa nini Nilitaka kusemezana na nyinyi kuhusu sentensi hii, “Mwana wa Adamu ni Bwana hata wa siku ya Sabato”? Maana yake ni kwamba kile kinachotoka kwa Mungu, kile Alichio nacho na kile Alichio, na kila kitu Chake vyote ni vikuu zaidi kuliko kitu kingine chochote, kikiwemo kile kitu au yule mtu ambaye uliwahi kuamini kuwa unamthamini zaidi. Hivyo ni kusema, kama mtu hawezi kupata maneno kutoka katika kinywa cha Mungu au kama haelewi mapenzi Yake, hawezi kupata pumziko. Katika yale mtakayopitia katika siku zako za usoni, mtaelewa ni kwa nini Nilitaka nyinyi kuona dondoo hii leo—hii ni muhimu sana. Kila kitu ambacho Mungu anafanya ni ukweli na maisha. Ukweli kwa mwanadamu ni kitu ambacho hawawezi kukosa katika maisha yao, kitu ambacho hawawezi kuishi bila; unaweza pia kusema kwamba ndicho kitu kikuu zaidi. Ingawa huwezi kukiangalia au kukigusa, umuhimu wake kwako hauwezi kupuuzwa; ndicho kitu cha pekee kinachoweza kukuletea pumziko moyoni mwako.

Je, ufahamu wenu wa ukweli umefungamana na hali yenu ya kibinafsi? Katika maisha halisi, lazima kwanza ufikirie ukweli upi unahusiana na watu, matukio, na vitu ambavyo umekumbana navyo; ni miongoni mwa ukweli huu ndimo unaweza kupata mapenzi ya Mungu na kuunganisha kile ulichokumbana nacho na mapenzi Yake. Iwapo hujui ni vipengele vipi vya ukweli vinavyohusiana na mambo ambayo umekumbana nayo lakini badala yake unaenda kwa njia ya moja kwa moja kutafuta mapenzi ya Mungu, huu ni mtazamo ambao hauna mwelekeo ambao hauwezi kufanikisha matokeo. Kama unataka kutafuta ukweli na kuelewa mapenzi ya Mungu, kwanza unahitaji kuangalia ni mambo ya aina gani ambayo yametendeka kwako, ni vipengele vipi vya ukweli ambavyo mambo hayo yana uhusiano navyo, na kisha uatafute ukweli maalum katika neno la Mungu ambalo linahusiana na kile ulichopitia. Kisha utafute njia ya matendo ambayo ni sahihi kwako katika ukweli huo; kutokana na njia hii unaweza kupata ufahamu usio wa moja kwa moja kuhusu mapenzi ya Mungu. Kutafuta na kutenda ukweli si kutumia kanuni au kufuata fomula bila kufikiria. Ukweli si wa kifomula, wala si sheria. Haujakufa—ni uzima wenyewe, ni kitu ambacho kina uhai, na ni kanuni ambayo lazima

kilichoumbwa kifuate katika Maisha na kanuni ambayo lazima mwanadamu awe nayo katika maisha yake. Hiki ni kitu ambacho lazima, kwa vyoyote vile, uelewe kupitia uzoefu. Haijalishi ni katika awamu gani ambayo umeifikia katika uzoefu wako, huwezi kutenganishwa na neno la Mungu au ukweli, na kile unachoelewa kuhusu tabia ya Mungu na kile unachojua kuhusu kile Alichacho Mungu na kile Alichacho ni vitu ambavyo vimeonyeshwa vyote katika maneno ya Mungu; vimeungana kabisa na ule ukweli. Tabia ya Mungu na kile Alichacho na kile Alichacho mwenyewe ni ukweli kwa njia yake; ukweli ni dhihirisho halisi la tabia ya Mungu na kile Alichacho na kile Alichacho. Unafanya kile Mungu Alichacho nacho kuonyesha waziwazi kile Mungu alisema; unakuonyesha moja kwa moja kile ambacho Mungu hapendi, kile ambacho Hapendi, kile Anachokutaka ufanye na kile ambacho Hakuruhusu ufanye, watu ambao Anawachukia na watu ambao Anawafurahia. Katika ule ukweli ambao Mungu anaonyesha watu wanaweza kuona furaha, hasira, huzuni, na shangwe Yake, pamoja na kiini Chake—huu ndio ufichuzi wa tabia Yake. Mbali na kujua kile Mungu Alichacho nacho na kile Alichacho, na kuelewa tabia Yake kutoka katika neno Lake, kile kilichomuhamu zaidi ni haja ya kufikia ufahamu huu kupitia kwa uzoefu wa kimatendo. Kama mtu atajiondoa katika maisha halisi ili kumjua Mungu, hataweza kutimiza hayo. Hata kama kuna watu wanaoweza kupata ufahamu fulani kutoka katika neno la Mungu, ufahamu wao umewekewa mipaka ya nadharia na maneno, na kunatokea tofauti na vile ambavyo Mungu alivyo mwenyewe kwa kweli.

Kile tunachozungumzia sasa kimo ndani ya ule upana wa hadithi zilizorekodiwa katika Biblia. Kupitia katika hadithi hizi, na kupitia uchambuzi wa mambo haya yaliyofanyika, watu wanaweza kuelewa tabia Yake na kile Alichacho nacho na kile Alichacho ambayo Ameonyesha, na kuwaruhusu kujua kila kipengele cha Mungu kwa upana zaidi, kwa kina zaidi, kikamilifu, na kwa undani zaidi. Hivyo basi, njia pekee ya kujua kila kipengele cha Mungu ni kupitia hadithi hizi? La, siyo! Kwani kile Mungu anachosema na kazi Anayofanya katika Enzi ya Ufalme kinaweza kuwasaidia watu kwa njia bora zaidi kujua tabia Yake, na kuijua kikamilifu. Hata hivyo, Nafikiri ni rahisi zaidi kujua tabia ya Mungu na kuelewa kile Alichacho nacho na kile Alichacho kupitia baadhi ya mifano au hadithi zilizorekodiwa katika Biblia ambazo watu wamezoeana nazo. Nikichukua maneno ya hukumu na kuadibu na ukweli ambao Mungu anaonyesha leo ili kukufanya umjue Yeye neno kwa neno, utahisi kwamba haipendezi sana inachosha mno, na baadhi ya watu hata watahisi kwamba maneno ya Mungu yanaonekana kuwa yanafuata fomula fulani. Lakini tukichukulia hadithi hizi za Biblia kama mifano ya kuwasaidia watu kujua tabia ya Mungu, basi haitaonekana kuwa ya kuchosha. Unaweza kusema kwamba katika mkondo wa kuonyesha mifano hii, maelezo ya kile kilichokuwa moyoni mwa Mungu wakati huo—hali Yake ya moyo au hisia Zake za moyoni, au fikira na mawazo Yake—vimesimuliwa kwa watu katika lugha za kibinadamu, na lengo la haya yote ni kuwaruhusu kushukuru, kuhisi kile Mungu Alichacho

nacho na kile Alichu na kujua kwamba si fomula. Si hadithi ya kale, au kitu ambacho watu hawawezi kuona wala kugusa. Ni kitu ambacho kwa kweli kipo ambacho watu wanaweza kuhisi, na kufahamu. Hili ndilo lengo la msingi. Unaweza kusema kwamba watu wanaoishi katika enzi hii wamebarikiwa. Wanaweza kuzitumia hadithi za Biblia kupata ufahamu mpana zaidi wa kazi za awali za Mungu; wanaweza kuona tabia Yake kupitia katika kazi ambayo Amefanya. Na wanaweza kuelewa mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu kupitia kwa tabia hizi ambazo Ameonyesha, kuelewa maonyesho yale thabiti ya utakatifu Wake na utunzaji Wake kwa binadamu ili kuweza kufikia maelezo zaidi na maarifa ya kina zaidi kuhusu tabia ya Mungu. Naamini kwamba nyinyi nyote mnaweza kuhisi haya yote!

Ndani ya upana wa kazi ambayo Bwana Yesu alikamilisha katika Enzi ya Neema, unaweza kuona kipengele kingine cha kile Alichu nacho Mungu na kile Alichu. Kilionyeshwa kupitia kwa mwili Wake, na kikawezeshwa kwa watu kuona na kufahamu zaidi kupitia kwa ubinadamu Wake. Ndani ya Mwana wa Adamu, watu waliweza kuona namna ambavyo Mungu katika mwili alivyoishi kwa kudhihirisha ubinadamu Wake, na wakaona uungu wa Mungu ulioonyeshwa kupitia kwa mwili. Aina hizi mbili za maonyesho ziliwaruhusu watu kuweza kumwona Mungu aliye halisi sana, na kuwaruhusu kuwa na dhana tofauti ya Mungu. Hata hivyo, katika kipindi cha muda kati ya uumbaji wa ulimwengu na mwisho wa Enzi ya Sheria, yaani, kabla ya Enzi ya Neema, kile kilichoonkana, kilichosikizwa, na kupitiwa na watu kilikuwa tu kipengele kitakatifu cha Mungu. Kilikuwa kile ambacho Mungu alifanya na kusema katika himaya ile isiyoshikika, na mambo ambayo Aliyaonyesha kutoka katika nafsi Yake halisi ambayo yasingeweza kuonekana au kuguswa. Mara nyingi, mambo haya yaliwafanya watu kuhisi kwamba Mungu alikuwa mkubwa sana, na kwamba wasingeweza kusonga karibu na Yeye. Picha ambayo Mungu kwa kawaida aliwapa watu ilikuwa kwamba Alionekana akipotea, na watu walihisi hata kwamba kila mojawapo ya fikira na mawazo Yake yalikuwa yenye mafumbo mno na yasiyoeleweka mno kiasi kwamba hakukuwa na njia ya kuyafikia, isitoshe hata kujaribu kuelewa na kuyashukuru. Kwa watu, kila kitu kuhusu Mungu kilikuwa cha mbali—mbali mno kiasi kwamba watu wasingeweza kukiona, wasingeweza kukigusa. Ilionekana Alikuwa juu katika mbingu, na ilionekana kwamba Hakukuwepo kamwe. Hivyo basi kwa watu, kuelewa moyo na akili ya Mungu au kufikiria Kwake kokote kusingeweza kutimizika, na hata kufikika. Ingawa Mungu alitenda kazi fulani thabiti katika Enzi ya Sheria, na Akaweza kutoa pia maneno fulani na kuonyesha tabia fulani mahususi ili kuwaruhusu watu kushukuru na kuona maarifa halisi fulani kumhusu, bado hatimaye, hilo lilikuwa ni maonyesho ya Mungu kuhusu Alichu nacho na kile Alichu katika ulimwengu usioshikika, na kile watu walielewa, kile walichojua kilikuwa bado kile cha kipengele takatifu kuhusu kile Alichu nacho na kile Alichu. Mwanadamu asingeweza kupata dhana thabiti kutoka kwa kile Alichu nacho na kile Alichu, na ile picha

waliyokuwa nayo kuhusu Mungu ilikuwa bado ndani ya mawanda ya “mwili wa kiroho” ulio mgumu kukaribia, unaoonekana na kupotea ndani na nje ya mtazamo.” Kwa sababu Mungu hakutumia kifaa mahususi au taswira katika ulimwengu wa kimwili kuonekana kwa watu, bado wasingeweza kumfafanua Yeye kwa kutumia lugha ya kibinadamu. Katika mioyo na akili za watu, siku zote walitaka kutumia lugha yao binafsi ili kuanzisha kiwango kwa ajili ya Mungu, kumfanya Agusike na kumfanya Awe binadamu, kama vile Alikuwa mrefu kiasi gani, Alikuwa mkubwa kiasi gani, Alifanana vipi, Anapenda nini hasa na hulka Yake mahususi ni gani. Kwa kweli, moyoni Mwake Mungu alijua kwamba watu walifikiria hivyo. Alikuwa wazi sana kuhusu mahitaji ya watu, na bila shaka Alijua pia kile Alichofaa kufanya, hivyo basi Alitenda kazi Yake kwa njia tofauti na Enzi ya Neema. Njia hii ilikuwa takatifu na vilevile iliyostaarabishwa. Katika kipindi cha Muda ambacho Bwana Yesu alikuwa akifanya kazi, watu wanguweza kuona kwamba Mungu alikuwa na maonyesho mengi ya kibinadamu. Kwa mfano, Aliweza kucheza, Aliweza kuhudhuria harusi, Aliweza kuwasiliana kwa karibu na watu, kuongea na wao, na kujadili mambo pamoja nao. Aidha, Bwana Yesu aliweza pia kukamilisha kazi nyingi zilizowakilisha uungu Wake, na bila shaka kazi Yake yote ilikuwa ni maonyesho na ufichuzi wa tabia ya Mungu. Katika kipindi hiki, wakati uungu wa Mungu ulitambuliwa kupitia kwa mwili wa kawaida ambao watu wanguweza kuona na kugusa, hawakuhisi tena kwamba Alikuwa akionekana na kutoweka, na kwamba wanguweza kumkaribia. Kinyume cha mambo ni kwamba, wangejaribu kuelewa mapenzi ya Mungu au kuuelewa uungu Wake kupitia kila hatua, maneno, na kazi ya Mwana wa Adamu. Mwana wa Adamu mwenye mwili alionyesha uungu wa Mungu kupitia kwa ubinadamu Wake na kuwasilisha mapenzi ya Mungu kwa binadamu. Na kupitia maonyesho ya mapenzi na tabia ya Mungu, Aliwafichulia watu yule Mungu asiyeweza kuonekana au kuguswa katika ulimwengu wa kiroho. Kile watu walichoona kilikuwa Mungu Mwenyewe, anayeshikika na aliye na mwili na mifupa. Hivyo basi Mwana wa Adamu mwenye mwili Alifanya mambo kama vile utambulisho binafsi wa Mungu, hadhi, taswira, tabia, na kile Alichacho na kile Alichacho kuwa thabiti na kupewa picha ya binadamu. Ingawa sura ya nje ya Mwana wa Adamu ilikuwa na upungufu fulani kuhusiana na taswira ya Mungu, kiini Chake na kile Alichacho na kile Alichacho yote hayo yaliweza kwa kikamilifu kuwakilisha utambulisho na hadhi binafsi ya Mungu—kulikuwa tu na tofauti fulani katika jinsi ya maonyesho. Bila kujali kama ni ubinadamu wa Mwana wa Mungu au uungu Wake, hatuwezi kukana kwamba Aliwakilisha utambulisho na hadhi binafsi ya Mungu mwenyewe. Katika kipindi hiki cha muda, hata hivyo, Mungu alifanya kazi kupitia mwili, Akaongea kutoka kwa mtazamo wa mwili, na kusimama mbele ya mwanadamu kwa utambulisho na hadhi ya Mwana wa Adamu, na hili liliwapa watu fursa ya kukumbana na kupitia maneno na kazi ya kweli ya Mungu miongoni mwa binadamu. Iliweza pia kuwaruhusu watu kuwa na utambuzi wa uungu Wake na ukubwa Wake katikati ya unyenyekevu, vilevile na kupata ufahamu wa mwanzo na ufafanuzi wa mwanzo wa

uhalali na uhalisi wa Mungu. Hata ingawa kazi iliyokamilishwa na Bwana Yesu, njia Zake za kufanya kazi, na mitazamo ambayo kutoka kwayo Aliongea ilitofautiana na ile ya nafsi halisi ya Mungu katika ulimwengu wa kiroho, kila kitu kumhusu kilimwakilisha kwa kweli Mungu Mwenyewe ambaye binadamu walikuwa hawajawahi kumwona awali—hili haliwezi kukataliwa! Hivi ni kusema, haijalishi ni kwa umbo gani ambalo Mungu huonekana, haijalishi huongea kutoka katika mtazamo upi, au Yeye hukabiliana na binadamu kupitia kwa taswira gani, Mungu hawakilishi chochote isipokuwa Yeye Mwenyewe. Hawezi kumwakilisha binadamu yeyote—Hawezi kumwakilisha binadamu yeyote aliyepotoka. Mungu ni Mungu Mwenyewe, na hili haliwezi kukataliwa.

Kifuatacho tutaangalia mfano uliozungumziwa na Bwana Yesu katika Enzi ya Neema.

3. Mfano wa Kondoo Aliyepotea

Mat 18:12-14 Mnafikiri vipi? Iwapo mtu ana kondoo mia moja, na mmoja wao apotee, je, hawaachi hao tisini na tisa, na kuenda milimani, na amtafute huyo ambaye amepotea? Na iwapo atampata, kweli nawaambia, anafurahi zaidi kwa sababu ya huyo kondoo, kuliko wao tisini na tisa ambao hawakupotea. Kwa namna hiyo siyo mapenzi ya Baba yenu ambaye yuko mbinguni, kuwa mmoja wa hawa wadogo aangamie.

Kifungu hiki ni fumbo—ni hisia gani watu wanapata kutokana fumbo hili? Namna ya kujieleza—fumbo—lilitumika hapa ni mbinu za lugha katika lugha ya binadamu, na kwa hivi ni kitu kilicho ndani ya mawanda ya maarifa ya binadamu. Kama Mungu angekuwa amesema kitu kinachofanana katika Enzi ya Sheria, watu wangehisi kwamba hakikuambatana na Alichokuwa Mungu, lakini Mwana wa Adamu alipoonyesha kifungu hiki katika Enzi ya Neema, kilionekana cha kufariji, chenye uzuri, na kilicho karibu kwa watu. Mungu alipokuwa mwili, Alipoonekana katika umbo la binadamu, Alitumia sitiari inayofaa sana kuonyesha sauti ya roho Yake katika ubinadamu. Sauti hii iliwakilisha sauti binafsi ya Mungu na kazi Aliyotaka kufanya katika enzi hiyo. Pia iliwakilisha mtazamo ambao Mungu alikuwa nao kwa watu katika Enzi ya Neema. Tukiangalia kutoka kwa mtazamo wa mwelekeo wa Mungu kwa watu, Alimfananisha kila mtu na kondoo. Kama kondoo amepotea, Atafanya kila awezalo ili kumpata. Hii inawakilisha kanuni ya kazi ya Mungu miongoni mwa binadamu wakati huu katika mwili. Mungu alitumia mfano huu kufafanua uamuzi na mwelekeo Wake katika kazi hiyo. Haya ndiyo yaliyokuwa manufaa ya Mungu kuwa mwili: Angeweza kutumia vizuri maarifa ya binadamu na kutumia lugha ya binadamu kuongea na watu, kuonyesha mapenzi Yake. Aliwaelezea au “kuwatafsiria” binadamu lugha Yake ya maana sana, ya kiungu ambayo watu walipata ugumu kuelewa kupitia lugha ya binadamu, kwa njia ya kibinadamu. Hii iliwasaidia watu kuelewa mapenzi Yake na kujua kile Alichotaka kufanya. Angeweza pia kuwa na mazungumzo na watu kutoka katika mtazamo wa

kibinadamu, kwa kutumia lugha ya kibinadamu, na kuwasiliana na watu kwa njia waliyoelewa. Aliweza pia kuongea na kufanya kazi kwa kutumia lugha na maarifa ya kibinadamu ili watu waweze kuhisi wema na ukaribu wa Mungu, ili wangeweza kuuona moyo Wake. Mnaona nini katika hili? Kwamba hakuna kuzuiliwa katika maneno na vitendo vya Mungu? Namna watu wanavyoona, hakuna njia ambayo Mungu angetumia maarifa ya kibinadamu, lugha, au njia za kuongea ili kuzungumza kuhusu kile ambacho Mungu Mwenyewe alitaka kusema, kazi Aliyotaka kufanya, au kuonyesha mapenzi Yake mwenyewe; huku ni kufikiria ambako si sahihi. Mungu alitumia aina hii ya sitiari ili watu waweze kuhisi ule uhalisi na uaminifu wa Mungu, na kuona mwelekeo Wake kwa watu katika kipindi hicho cha muda. Mfano huu uliwazindua watu waliokuwa wakiishi chini ya sheria kwa muda mrefu kutoka katika ndoto, na vilevile uliweza kuhemsha kizazi baada ya kizazi cha watu walioishi katika Enzi ya Neema. Kwa kukisoma kifungu cha mfano huu, watu wanajua uaminifu wa Mungu katika kuwaokoa binadamu na wanaelewa uzito wa mwanadamu katika moyo Wake.

Hebu tuangalie kwa mara nyingine sentensi ya mwisho katika dondoo hii: “Kwa namna hiyo siyo mapenzi ya Baba yenu ambaye yuko mbinguni, kuwa mmoja wa hawa wadogo aangamie.” Haya yalikuwa maneno binafsi ya Bwana Yesu, au yalikuwa maneno ya Baba Yake aliye mbinguni? Kwa juujuu, yaonekana alikuwa Bwana Yesu akiongea, lakini mapenzi Yake yanawakilisha mapenzi ya Mungu Mwenyewe, na ndiyo maana Akasema: “Kwa namna hiyo siyo mapenzi ya Baba yenu ambaye yuko mbinguni, kuwa mmoja wa hawa wadogo aangamie.” Watu wakati huo walimtambua tu Baba aliye mbinguni kama Mungu, na mtu huyu waliyeona mbele ya macho yao alikuwa ametumwa tu na Yeye, na hakuweza kuwakilisha Baba aliye mbinguni. Ndiyo maana Bwana Yesu alilazimika kusema hivyo vilevile, ili waweze kuhisi kwa kweli mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu, na kuhisi ule uhalali na usahihi wa kile Alichosema. Hata ingawa jambo hili lilikuwa jepesi kusema, lilikuwa lenye utunzaji mwingi na lilifichua unyenyekevu na ufiche wa Bwana Yesu. Bila kujali kama Mungu alikuwa mwili au Alifanya kazi katika ulimwengu wa kiroho, Alijua moyo wa binadamu kwa njia bora zaidi, na Alielewa kwa njia bora zaidi kile watu walichohitaji, Alijua ni nini watu walikuwa na wasiwasi kuhusu, na kile kilichowakanganya, hivyo Akaongeza mstari huu. Mstari huu uliangazia tatizo lililofichika ndani ya mwanadamu: Watu hawakuamini kile ambacho Mwana wa Adamu alisema, hivi ni kusema kwamba, Bwana Yesu alipokuwa akiongea Alilazimika kuongeza: “Kwa namna hiyo siyo mapenzi ya Baba yenu ambaye yuko mbinguni, kuwa mmoja wa hawa wadogo aangamie.” Ni katika kauli hii tu ndiyo maneno Yake yangezaa matunda, kuwafanya watu kuamini usahihi wao na kuboresha kiwango cha kuaminika kwa maneno hayo. Hii inaonyesha kwamba Mungu alipokuwa Mwana wa Adamu wa kawaida, Mungu na mwanadamu walikuwa na uhusiano mgumu sana, na kwamba hali ya Mwana wa Adamu ilikuwa ya kuaibisha mno. Inaonyesha pia

namna ambavyo hadhi ya Bwana Yesu ilivyokuwa isiyo na maana miongoni mwa binadamu wakati huo. Aliposema haya, kwa hakika ilikuwa ni kuwaambia watu: Mnaweza kuwa na uhakika kwamba—haya hayawakilishi yale yaliyo moyoni Mwangu mwenyewe, lakini ni mapenzi ya Mungu aliye mioyoni mwenu. Kwa mwanadamu, jambo hili halikuwa la kejeli? Ingawa Mungu kufanya kazi katika mwili kulikuwa na manufaa mengi ambayo Hakuwa nayo katika nafsi Yake, Alilazimika kustahimili shaka na kukataliwa na wao pamoja na kutojali na kutochangamka kwao. Yaweza kusemekana kwamba mchakato wa kazi ya Mwana wa Adamu ulikuwa mchakato wa kupitia kukataliwa na mwanadamu, na kuhisi mashindano yao akishindana dhidi Yake. Zaidi ya hayo, ulikuwa ni mchakato wa kufanya kazi ili kuendelea kushinda imani ya mwanadamu na kumshinda mwanadamu kupitia kile Alichu nacho na kile Alichu, kupitia kiini Chake binafsi halisi. Haikuwa sana kwamba Mungu mwenye mwili Alikuwa akipigana vita vikali dhidi ya Shetani; ilikuwa zaidi kwamba Mungu aligeuka na kuwa binadamu wa kawaida na kuanzisha mapambano pamoja na wale wanaomfuata Yeye, na katika mapambano haya Mwana wa Adamu alikamilisha kazi Yake kwa unyenyekevu Wake, pamoja na kile Alichu nacho na kile Alichu, na upendo na hekima Yake. Aliwapata watu Aliowataka, kushinda utambulisho na hadhi Aliyostahili, na “kurudi” kwa kiti Chake cha enzi.

Kifuatacho, hebu basi tuangalie dondoo mbili zifuatazo katika maandiko.

4. Samehe Sabini Mara Saba

Mat 18:21-22 Kisha Petro akakuja kwake, na kusema, Bwana, ni mara ngapi ndugu yangu atanikosea, nami nimsamehe? Hadi mara saba? Yesu akasema kwake, sikuambii, hadi mara saba: ila, hadi sabini mara saba.

5. Upendo wa Bwana

Mat 22:37-39 Yesu akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako mzima, na roho yako nzima, na akili yako nzima. Hii ni amri ya kwanza na kubwa. Na ya pili ni kama hiyo, Mpende jirani yako kama unavyojipenda.

Kati ya dondoo hizi mbili, moja yazungumzia msamaha na nyingine inazungumzia upendo. Mada hizi mbili zinaangazia kwa kweli kazi ambayo Bwana Yesu alitaka kutekeleza katika Enzi ya Neema.

Wakati Mungu alipokuwa mwili, Alileta pamoja naye hatua ya kazi Yake—Alileta pamoja naye kazi mahususi na tabia Aliyotaka kuonyesha katika enzi hii. Katika kipindi hicho, kila kitu ambacho Mwana wa Adamu alifanya kilizungukia kazi ambayo Mungu alitaka kutekeleza katika enzi hii. Asingeweza kufanya zaidi au kufanya kidogo zaidi. Kila kitu Alichosema na kila aina

ya kazi Aliyotekeleza ilihusiana yote na enzi hii. Haijalishi kama Alionyesha kwa njia ya kibinadamu Akitumia lugha ya kibinadamu au kupitia kwa lugha ya kiungu—haijalishi ni njia gani, au kutoka kwa mtazamo gani—lengo Lake lilikuwa ni kuwasaidia watu kuelewa kile Alichotaka kufanya, mapenzi Yake yalikuwa nini, na mahitaji Yake yalikuwa yapi kutoka kwa watu. Anaweza kutumia mbinu mbalimbali kutoka mitazamo mbalimbali ili kuwasaidia watu kuelewa na kujua mapenzi Yake, kuelewa kazi Yake ya kuwaokoa binadamu. Hivyo basi katika Enzi ya Neema tunamwona Bwana Yesu akitumia lugha ya kibinadamu wakati mwingi kuonyesha kile Alichotaka kuwasilisha kwa mwanadamu. Hata zaidi, tunamwona kutoka katika mtazamo wa mwelekezi wa kawaida Akiongea na watu, Akishughulikia mahitaji yao, na Akiwasaidia na kile walichoomba. Njia hii ya kufanya kazi haikuonekana katika Enzi ya Sheria iliyokuja kabla ya Enzi ya Neema. Aligeuka na kuwa karibu zaidi na mwenye huruma zaidi kwa binadamu, pamoja na kuweza kutimiza zaidi matokeo ya kimatendo katika umbo Lake na tabia Yake. Istiara kuhusu kusamehe watu sabini mara saba unafafanua zaidi hoja hii. Kusudio lililotimizwa kupitia kwa nambari katika Istiara hii ni kuwaruhusu watu kuelewa nia ya Bwana Yesu wakati huo aliposema hayo. Nia Yake ilikuwa kwamba watu wanafaa kuwasamehe wengine—si mara moja wala mara mbili na wala si hata mara saba, lakini sabini mara saba. Hili wazo la “sabini mara saba” ni la aina gani? Ni la kuwafanya watu kufanya msamaha kuwa wajibu wao wa kibinafsi, kitu ambacho lazima wajifunze, na “njia” ambayo kwayo ni lazima waishi. Hata ingawa hii ilikuwa Istiara tu, iliwasaidia watu kufahamu kwa kina. Ilisaidia pwatu kutafuta njia bora za kufanyia mazoezi na kanuni na viwango vya utendaji. Istiara hii iliwasaidia watu kuweza kuelewa waziwazi na ikawapa wazo sahihi—kwamba wanafaa kujifunza kusamehe na wasamehe nambari yote bila ya masharti na bila ya upungufu wowote, lakini kwa mtazamo wa uvumilivu na ufahamu kwa wengine. Bwana Yesu aliposema haya, ni nini kilichokuwa moyoni Mwake? Alikuwa akifikiria kwa kweli kuhusu sabini mara saba? Hakuwa akifikiri kuhusu hilo. Ipo idadi ya mara ambazo Mungu atawasamehe binadamu? Kunao watu wengi walio na shauku katika “idadi” iliyotajwa, wanaotaka kwa kweli kuelewa asili na maana ya nambari hii. Wanataka kuelewa kwa nini nambari hii ilitoka kinywani mwa Bwana Yesu; wanaamini kwamba kuna uhusisho wa kina zaidi katika nambari hii. Kwa hakika, huu ulikuwa ni usemi tu wa Mungu katika ubinadamu. Uhusisho au maana yoyote lazima ichukuliwe pamoja na mahitaji ya Bwana Yesu kwa mwanadamu. Wakati Mungu alikuwa bado hajawa mwili, watu hawakuelewa mengi ya Alichosema kwa sababu kilitoka katika uungu kamilifu. Mtazamo na muktadha wa kile Alichosema ulikuwa hauonekani na haufikiwi na mwanadamu; ulionyesha kutoka katika ulimwengu wa kiroho ambayo watu wasingeweza kuiona. Kwa watu walioishi katika mwili, wasingeweza kupita katika ulimwengu wa kiroho. Lakini baada ya Mungu kuwa mwili, Aliongea na mwanadamu kutoka katika mtazamo wa ubinadamu, na Alitoka kwa na, na akazidi mawanda ya ulimwengu wa kiroho. Angeweza kuonyesha tabia Yake ya uungu,

mapenzi, na mtazamo, kupitia mambo yale ambayo binadamu wangeweza kufikiria na mambo yale wangeweza kuona na kukumbana nayo katika maisha yao, kwa kutumia mbinu ambazo binadamu wangeweza kukubali, kwa lugha ambayo wangeweza kuelewa, na maarifa ambayo wangeweza kuelewa, ili kuruhusu mwanadamu kumwelewa na kumjua Mungu, kufahamu nia Yake na viwango Vyake hitajika ndani ya mawanda ya uwezo wao; hadi kufikia kiwango ambacho wangeweza. Hii ndiyo iliyokuwa mbinu na kanuni ya kazi ya Mungu kwa ubinadamu. Ingawa njia za Mungu na kanuni Zake za kufanya kazi katika mwili ziliweza kutimizwa sana kwa, au kupitia kwa ubinadamu, ziliweza kwa kweli kutimiza matokeo ambayo yasingeweza kutimizwa kwa kufanya kazi moja kwa moja katika uungu. Kazi ya Mungu katika ubinadamu ilikuwa thabiti zaidi, halisi, na yenye malengo, mbinu zilikuwa zaweza kubadilika kwa urahisi zaidi, na kwa umbo iliweza kupita Enzi ya Sheria.

Hapa chini, hebu tuzungumzie kumpenda Bwana na kumpenda jirani yako kama unavyojipenda. Je, hili ni jambo linaloelezewa moja kwa moja kupitia uungu? Bila shaka silo! Haya yalikuwa mambo yote ambayo Mwana wa Adamu alisema kwa ubinadamu; watu tu ndio wangeweza kusema kauli kama “Mpende jirani yako kama unavyojipenda. Kuwapenda wengine ni sawa na kuyatunza maisha yako binafsi,” na watu tu ndio wangeweza kuongea kwa njia hii. Mungu hajawahi kuongea kwa njia hiyo. Kwa kiwango cha chini zaidi, Mungu hana aina hii ya lugha katika uungu Wake kwa sababu Hahitaji aina hii ya imani, “Mpende jirani yako kama unavyojipenda” ili kudhibiti upendo Wake kwa mwanadamu, kwa sababu upendo wa Mungu kwa mwanadamu ni ufichuzi wa kiasili wa kile Alichu nacho na kile Alichu. Ni lini mmewahi kusikia kwamba Mungu alisema kitu kama “Nampenda binadamu kama Ninavyojipenda”? Kwa sababu upendo umo katika kiini cha Mungu, na ndani ya kile Alichu nacho na kile Alichu. Upendo wa Mungu kwa binadamu na jinsi Anavyowashughulikia watu na mtazamo Wake ni maonyesho ya kiasili na ufichuzi wa tabia Yake. Hahitaji kufanya hili kwa njia fulani kimakusudi, au kufuata mbinu fulani au mfumo wa maadili kimakusudi ili kutimiza kumpenda jirani Yake kama Anavyojipenda—tayari Anamiliki aina hii ya kiini. Unaona nini katika haya? Wakati Mungu alipofanya kazi katika ubinadamu, mbinu, maneno, na ukweli Wake mwingi vyote vilionyeshwa kwa njia ya kibinadamu. Lakini wakati uo huo tabia ya Mungu, kile Alichu nacho na kile Alichu, na mapenzi Yake vyote vilionyeshwa kwa watu kuweza kujua na kuvielewa. Kile walichojua na kuelewa kilikuwa hasa kiini Chake na Alichu nacho na kile Alichu, vyote ambavyo vinawakilisha utambulisho na hadhi ya asili ya Mungu Mwenyewe. Hivyo ni kusema kwamba, Mwana wa Adamu kwa mwili Alionyesha tabia ya asili na kiini cha Mungu Mwenyewe kwa kiwango kikubwa zaidi kinachowezekana na kwa usahihi zaidi unaowezekana. Ubinadamu wa Mwana wa Adamu haukuwa pingamizi au kizuizi cha mawasiliano na kuingiliana kwa binadamu na Mungu mbinguni tu, bali kwa hakika ilikuwa ndio

njia ya pekee na daraja la pekee la mwanadamu kuungana na Bwana wa uumbaji. Wakati huu, je, hamhisi kwamba kunayo mifanano mingi kati ya asili na mbinu za kazi iliyofanywa na Bwana Yesu katika Enzi ya Neema na awamu ya sasa ya kazi? Hatua ya sasa ya kazi inatumia pia lugha nyingi za kibinadamu kueleza tabia ya Mungu, na inatumia lugha na mbinu nyingi kutoka katika maisha ya kila siku ya binadamu na maarifa ya kibinadamu ili kuonyesha mapenzi binafsi ya Mungu. Punde Mungu anapokuwa mwili, haijalishi kama Anaongea kutoka kwa mtazamo wa kibinadamu au mtazamo wa kiungu, wingi wa lugha na mbinu Zake za maonyesho yote ni kupitia katika njia ya lugha na mbinu za kibinadamu. Yaani, wakati Mungu anapokuwa mwili, ndiyo fursa bora zaidi ya wewe kuweza kuona kudura ya Mungu na hekima Yake, na kujua kila kipengele halisi cha Mungu. Mungu alipogeuka na kuwa mwili, wakati Alikuwa Akikua, Alipata kuelewa, kujifunza, na kuelewa baadhi ya maarifa ya binadamu, maarifa ya kawaida, lugha, na mbinu za maonyesho katika ubinadamu. Mungu mwenye mwili alimiliki mambo haya yaliyotokana na binadamu Aliyekuwa ameumba. Waligeuka na kuwa zana za Mungu katika mwili za kueleza tabia Yake na uungu Wake, na wakamruhusu kuifanya kazi Yake ya kufaa zaidi, halisi zaidi, na sahihi zaidi Alipokuwa akifanya kazi katikati ya mwanadamu, kutoka katika mtazamo wa kibinadamu na kwa kutumia lugha ya kibinadamu. Iliiwezesha kufikiwa zaidi na kueleweka kwa urahisi zaidi na watu, hivyo basi kutimiza matokeo ya kile Mungu Alichotaka. Je, si jambo la busara zaidi kwa Mungu kufanya kazi kupitia kwa mwili kwa njia hii? Je, hii sio hekima ya Mungu? Wakati Mungu alipogeuka na kuwa mwili, wakati mwili wa Mungu uliweza kuchukua kazi Aliyotaka kutekeleza, ndipo Angeonyesha tabia Yake na kazi Yake kwa utendaji, na huu ndio wakati pia ambao Angeanza rasmi huduma Yake kama Mwana wa Adamu. Hii ilimaanisha kwamba hakukuwepo tena pengo la kizazi kati ya Mungu na binadamu, kwamba Mungu angesitisha karibuni kazi Yake ya kuwasiliana kupitia kwa wajumbe, na kwamba Mungu Mwenyewe binafsi angeweza kuonyesha maneno na kazi zote Alizotaka kufanya katika mwili. Hii ilimaanisha pia kwamba watu ambao Mungu huokoa walikuwa karibu na Yeye, na kwamba kazi Yake ya usimamizi ilikuwa imeingia eneo jipya, na kwamba binadamu wote walikuwa karibu kukumbwa na enzi mpya.

Kila mtu ambaye amesoma Biblia anajua kwamba mambo mengi yalifanyika Bwana Yesu alipozaliwa. Kubwa zaidi miongoni mwa hayo lilikuwa kutafutwa na mfalme wa ibilisi, hadi kufikia kiwango cha watoto wote wenye umri wa miaka miwili na chini katika eneo hilo kuchinjwa. Ni dhahiri kwamba Mungu alichukua hatari kubwa kwa kuwa mwili miongoni mwa binadamu; gharama kubwa Aliyolipia kwa ajili ya kukamilisha usimamizi Wake wa kumwoko mwanadamu pia ni wazi. Matumaini makubwa ambayo Mungu alishikilia kwa ajili ya kazi Yake miongoni mwa wanadamu katika mwili pia ni wazi. Wakati mwili wa Mungu uliweza kuchukua kazi miongoni mwa wanadamu, Alikuwa anahisi vipi? Watu wanafaa kuweza kuelewa hilo

kidogo, sivyo? Kwa kiwango cha chini zaidi, Mungu alifurahia kwa sababu Angeanza kuendeleza kazi Yake mpya miongoni mwa wanadamu. Bwana Yesu alipobatizwa na kuanza rasmi kazi Yake kukamilisha huduma Yake, moyo wa Mungu ulijawa na furaha kwa sababu baada ya miaka mingi sana ya kusubiri na matayarisho, hatimaye Angeweza kuuvaa mwili wa binadamu wa kawaida na kuanza kazi Yake mpya katika umbo la binadamu aliye na mwili na damu ambao watu wangeweza kuona na kugusa. Angeweza kuzungumza ana kwa ana na moyo kwa moyo na watu kupitia utambulisho wa binadamu. Mungu hatimaye angeweza kuwa ana kwa ana na mwanadamu katika lugha ya kibinadamu, kwa njia ya kibinadamu; Angeweza kumruzuku mwanadamu, kumwelimisha binadamu, na kumsaidia binadamu kwa kutumia lugha ya kibinadamu; angeweza kula kwenye meza moja na kuishi katika nafasi sawa na binadamu. Angeweza pia kuwaona binadamu, kuona vitu, na kuona kila kitu kwa njia ambayo binadamu walifanya hivyo na hata kupitia kwa macho yao. Kwake Mungu, huu ulikuwa tayari ushindi Wake wa kwanza wa kazi Yake katika mwili. Yaweza pia kusemekana kwamba yalikuwa ni ufanikishaji wa kazi kubwa—hili bila shaka ndilo ambalo Mungu alilifurahia zaidi. Kuanzia hapo ndiyo mara ya kwanza ambayo Mungu alihisi tulizo fulani katika kazi Yake miongoni mwa wanadamu. Matukio haya yote yalikuwa ya kimatendo sana na ya asili sana, na tulizo ambalo Mungu alihisi lilikuwa halisi. Kwa mwanadamu, kila mara hatua mpya ya kazi ya Mungu inapokamilishwa, na kila mara Mungu anapohisi kuridhika, ndipo mwanadamu anapoweza kusogea karibu zaidi na Mungu, na ndipo watu wanapoweza kusonga karibu zaidi na wokovu. Kwa Mungu, huu pia ni uzinduzi wa kazi Yake mpya, wakati mpango Wake wa usimamizi unapoendelea hatua moja zaidi, na, aidha, wakati mapenzi Yake yanapokaribia mafanikio kamili. Kwa mwanadamu, kuwasili kwa fursa kama hiyo ni bahati, na nzuri sana; kwa wale wote wanaosubiria wokovu wa Mungu, ni kubwa na habari za furaha. Mungu anapotekeleza hatua mpya ya kazi, basi Anao mwanzo mpya na wakati ambapo kazi hii mpya na mwanzo mpya vinazinduliwa na kufahamishwa miongoni mwa binadamu, ni wakati ambao matokeo ya hatua hii ya kazi tayari yameamuliwa, na kufanikishwa, naye Mungu tayari ameona athari yake ya mwisho na tunda. Huu pia ndio wakati ambapo athari hizi zinamfanya Mungu aridhike, na moyo Wake, bila shaka una furaha. Kwa sababu katika macho ya Mungu, tayari ameona na kuamua watu anaowatafuta, na tayari Amelipata kundi hili, kundi ambalo linaweza kufanya kazi Yake kufanikiwa na kumpa utoshelevu, Mungu anahisi Akiwa ameondolewa shaka, Anaweka pembeni wasiwasi Wake, na Anahisi mwenye furaha. Kwa maneno mengine, wakati mwili wa Mungu unaweza kuanza kazi mpya miongoni mwa binadamu, na Anaanza kufanya kazi ambayo lazima Afanye bila ya kizuizi, na wakati Anapohisi kwamba yote yamefanikishwa, tayari Ameuona mwisho. Na kwa sababu ya mwisho huu Anatosheka, na kuwa mwenye moyo wa furaha. Furaha ya Mungu inaonyeshwa vipi? Unaweza kufikiria jawabu litakuwa lipi? Je, Mungu anaweza kulia? Mungu Anaweza kulia? Mungu Anaweza kupiga makofi? Mungu Anaweza kucheza?

Mungu Anaweza kuimba? Na wimbo huo ungekuwa upi? Bila shaka Mungu Angeweza kuimba wimbo mzuri, wa kisisimua, wimbo ambao unaweza kuonyesha shangwe na furaha katika moyo Wake. Angeweza kuwaimbia binadamu, kujiambia Mwenyewe, na kuuimba kwa viumbe vyote. Furaha ya Mungu inaweza kuonyeshwa kwa njia yoyote—yote haya ni kawaida kwa sababu Mungu ana shangwe na huzuni, na hisia Zake mbalimbali zinaweza kuonyeshwa kwa njia mbalimbali. Hii ndiyo haki Yake na hakuna kitu kingekuwa cha kawaida zaidi na sahihi. Watu hawafai kufikiria chochote kingine kuhusu hili. Hufai kujaribu kutumia “laana ya kukzana mshipi”^[a] kwa Mungu, ukimwambia kwamba Yeye hafai kufanya hiki au kile, Hafai kutenda kwa njia hii au ile, kuwekea mipaka shangwe Yake au hisia yoyote ile Aliyo nayo. Katika mioyo ya watu Mungu hawezi kuwa na furaha, Hawezi kutokwa na machozi, Hawezi kulia—Hawezi kuonyesha hisia zozote. Kupitia yale tuliyowasiliana katika nyakati hizi mbili, Naamini hamtamwona tena Mungu kwa njia hii, lakini mtamruhusu Mungu kuwa na uhuru na uachiliaji fulani. Hiki ni kitu kizuri. Katika siku za usoni kama mtaweza kuhisi kwa kweli huzuni ya Mungu mnaposikia kwamba Yeye ana huzuni, na mnaweza kuhisi kwa kweli shangwe Yake mnaposikia kuhusu Yeye kuwa na furaha—angalau, mnaweza kujua na kuelewa waziwazi kile kinachomfanya Mungu kuwa na furaha na kile kinachomfanya Yeye kuwa na huzuni—unapoweza kuhisi huzuni kwa sababu Mungu ana huzuni na kuhisi furaha kwa sababu Mungu ana furaha, Atakuwa ameupata moyo wako na hakutakuwa tena na kizuizi chochote na Yeye. Hamtajaribu tena kumzuilia Mungu na fikira na maarifa ya binadamu. Wakati huo, Mungu atakuwa hai na dhahiri moyoni mwako. Atakuwa Mungu wa maisha yako na Bwana wa kila kitu chako. Je, mnalo tamanio kama hili? Je, mnayo imani kuwa mnaweza kutimiza haya?

Halafu hebu tusome fahamu zifuatazo.

6. Ibada Mlimani

Sifa na Heri (Mat 5:3-12)

Chumvi na Nuru (Mat 5:13-16)

Sheria (Mat 5:17-20)

Kuhusu Hasira (Mat 5:21-26)

Kuhusu Uzinzi (Mat 5:27-30)

Kuhusu Talaka (Mat 5:31-32)

Kuhusu Viapo (Mat 5:33-37)

Kuhusu Kulipiza Kisasi (Mat 5:38-42)

Upendo kwa Adui (Mat 5:43-48)

Kuhusu Utoaji Sadaka (Mat 6:1-4)

Kuhusu Maombi (Mat 6:5-8)

7. Mifano ya Bwana Yesu

Mfano wa Mpanzi (Mat 13:1-9)

Mfano wa Magugu katikati ya Ngano (Mat 13:24-30)

Mfano wa Punje ya Haradali (Mat 13:31-32)

Mfano wa Chachu (Mat 13:33)

Mfano wa Magugu Umeelezwa (Mat 13:36-43)

Mfano wa Hazina (Mat 13:44)

Mfano wa Lulu (Mat 13:45-46)

Mfano wa Wavu (Mat 13:47-50)

8. Amri

Mat 22:37-39 Yesu akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako mzima, na roho yako nzima, na akili yako nzima. Hii ni amri ya kwanza na kubwa. Na ya pili ni kama hiyo, Mpende jirani yako kama unavyojipenda.

Hebu kwanza tuangalie katika kila sehemu ya “Ibada Mlimani.” Haya yote yanahusiana na nini? Yaweza kusemekana kwa uhakika kwamba haya yote yameinuliwa zaidi, yana uthabiti zaidi na karibu zaidi katika maisha ya watu kuliko taratibu zile za Enzi ya Sheria. Kuzungumza katika muktadha wa kisasa, yanahusiana zaidi na matendo halisi ya watu.

Hebu tusome maudhui mahususi ya yafuatayo: Mnafaa kuzielewa vipi hali hizi za heri? Ni nini mnachofaa kujua kuhusu sheria? Ghadhabu inafaa kufasiliwa vipi? Wazinzi wanafaa kushughulikiwa vipi? Ni nini kinachosemwa, na ni sheria aina gani zipo kuhusu talaka, na ni nani anayeweza kutalikiwa na ni nani asiyeweza kutalikiwa? Na je, viapo, jicho kwa jicho, kuwapenda adui zako, maagizo kuhusu sadaka? Na kadhalika Mambo haya yote yanahusu kila kipengele cha matendo ya imani ya mwanadamu kwa Mungu, na ufuataji wao wa Mungu. Baadhi ya desturi hizi zinatumiwa leo, lakini bado yapo katika hali ya kimsingi kuliko mahitaji ya sasa ya watu. Kwa kiasi kikubwa uko katika hali ya kimsingi ambao watu wanakumbana nao

katika kuamini kwao katika Mungu. Tangu wakati Bwana Yesu alianza kufanya kazi, Alikuwa tayari anaanza kufanya kazi kwa tabia ya maisha ya binadamu, lakini yalitokana na msingi wa sheria. Je, sheria na misemo kuhusu mada hizi ilikuwa na uhusiano wowote na ukweli? Bila shaka zilikuwa nao! Taratibu, kanuni na ibada zote zingine za awali katika Enzi ya Neema zilikuwa na uhusiano, na tabia ya Mungu na kile Alichacho na kile Alichacho na bila shaka kwa ukweli. Haijalishi ni nini ambacho Mungu anaonyesha, kwa njia gani Anaonyesha, au Akitumia lugha gani, asili yake, na mwanzo wake, vyote vinatokana na kanuni za tabia Yake na kile Alichacho na kile Alichacho. Hili halina kosa. Kwa hivyo ingawa haya mambo Aliyoyasema yanaonekana kuwa ya juujuu, bado hamwezi kusema kwamba mambo haya si ukweli, kwa sababu yalikuwa mambo ambayo yalikuwa ya lazima kwa watu katika Enzi ya Neema ili kuridhisha mapenzi ya Mungu na kutimiza mabadiliko katika tabia yao ya maisha. Unaweza kusema kwamba mambo yoyote yale katika ibada hayaambatani na ukweli? Huwezi! Kila mojawapo ya mambo haya ni ukweli kwa sababu yote yalikuwa mahitaji ya Mungu kwa mwanadamu; yote yalikuwa kanuni na mawanda yaliyotolewa na Mungu kuhusu namna ambavyo unaweza kuwa na mwenendo, na yanawakilisha tabia ya Mungu. Hata hivyo, kutokana na kiwango cha ukuaji wao katika maisha wakati huo, waliweza tu kukubali na kuyafahamu mambo haya. Kwa sababu dhambi ya mwanadamu ilikuwa bado haijatatuliwa, Bwana Yesu angeweza tu kuyatoa maneno haya, na Angeweza kutumia mafundisho mepesi kama hayo miongoni mwa aina hii ya upana ili kuwaambia watu wa wakati huo namna ambavyo walifaa kutenda, kile walichofaa kufanya, ndani ya kanuni na upana gani walifaa kufanya mambo, na vipi walivyofaa kuamini katika Mungu na kutimiza mahitaji Yake. Haya yote yaliambiwa kulingana na kimo cha mwanadamu wakati huo. Haikuwa rahisi kwa watu wanaoishi katika sheria kuyakubali mafundisho haya, hivyo basi kile Alichofunza Bwana Yesu lazima kingebaki ndani ya mawanda haya.

Halafu, hebu tuangalie ni nini kilicho katika “Mifano ya Bwana Yesu.”

Mfano wa kwanza ni mfano wa mpanzi. Huu ni mfano wa kuisimua kweli; upanzi wa mbegu ni tukio maarufu sana katika maisha ya watu. Mfano wa pili ni mfano wa magugu. Kulingana na jinsi magugu yalivyo, yeyote ambaye amewahi kupanda mimea na watu wazima watajua. Wa tatu ni mfano wa punje ya haradali. Nyinyi nyote mnajua haradali ni nini, sivyo? Kama hujui, unaweza kupekua pekua katika Biblia. Nao mfano wa nne ni mfano wa chachu, watu wengi wanajua kwamba chachu inatumiwa katika kutia chachu; ni kitu ambacho watu wanatumia katika maisha yao ya kila siku. Mifano yote iliyotajwa hapa chini ukiwemo mfano wa sita, mfano wa hazina, mfano wa saba, mfano wa lulu, na wa nane mfano wa wavu; ni mifano iliyotolewa katika maisha ya watu; inatoka katika maisha ya watu halisi. Ni picha ya aina gani inayoonyeshwa na mifano hii? Hii ni picha ya Mungu akigeuka kuwa mtu wa kawaida na kuishi

pamoja na mwanadamu, Akitumia lugha ya maisha ya kila siku, Akitumia lugha ya mwanadamu ili kuwasiliana na binadamu na kuwapa kile wanachohitaji. Wakati Mungu alikuwa mwili na kuishi miongoni mwa wanadamu kwa muda mrefu, baada ya kupitia na kushuhudia hali ya maisha mbalimbali ya watu, hali hii Aliyopitia kilikuwa kitabu Chake cha kiada cha kubadilisha lugha Yake ya kiungu kuwa lugha ya binadamu. Bila shaka, mambo haya Aliyoyaona na kuyasikia katika maisha yaliweza pia kumwimarisha Mwana wa Adamu kupitia yale Aliyopitia akiwa binadamu. Alipowataka watu waelewe ukweli fulani, ili kuwaelewesha mapenzi fulani ya Mungu, Angetumia mifano inayofanana na ile iliyotajwa hapo juu ili kuwaeleza watu kuhusu mapenzi ya Mungu na mahitaji Yake kwa binadamu. Mifano hii yote ilihusiana na maisha ya watu; hakukuwa na hata mmoja ambao haukuwa na mguso wa maisha ya binadamu. Bwana Yesu alipoishi na binadamu, Aliwaona wakulima wakilima mashamba yao; Alijua magugu yalikuwa nini na kutia chachu kulikuwa nini; Alielewa kwamba binadamu wanapenda hazina na hivyo basi Alitumia sitiari za hazina na hata lulu. Kwa mjibu wa Maisha mara kwa mara Aliwaona wavuvi wakizirusha nyavu zao na kadhalika; Bwana Yesu alizona hizi na shughuli zingine zilizo na uhusiano na maisha ya wanadamu, Akipitia milo mitatu kwa siku ya binadana pia alipitia shughuli za kawaida za kila siku na kula mara tatu kwa siku. Aliweza kupitia kibinafsi maisha ya mtu wa kawaida na akashuhudia maisha ya wengine. Aliposhuhudia na kupitia haya yote binafsi, kile Alichofikiria kilikuwa si namna ya kuwa na maisha mazuri au namna ambavyo Angeishi kwa uhuru zaidi au kwa utulivu zaidi. Alipokuwa akipitia maisha halisi ya binadamu, Bwana Yesu aliuona ugumu katika maisha ya watu, Aliuona ugumu, ule ufukara, huzuni ya watu waliopotoshwa na Shetani, wakiishi katika utawala wa Shetani na walioishi katika dhambi. Huku akiyapitia maisha ya binadamu, Yeye binafsi aliweza pia kushuhudia namna ambavyo watu waliokuwa wakiishi ndani ya upotovu walivyokuwa wasioweza kujisaidia, na Akawaona kupitia ile hali duni ya wale walioishi katika dhambi, wale waliopotea katika mateso ya Shetani, ya mwovu. Bwana Yesu alipoyaona mambo haya, Aliyaona kwa macho Yake ya uungu au macho Yake ya ubinadamu? Ubinadamu Wake ulikuwepo kwa kweli—ulikuwepo waziwazi—Angeweza kuyapitia na kuyaona haya yote na bila shaka Aliyaona katika kiini Chake halisi, katika uungu Wake. Yaani, Kristo Mwenyewe, Bwana Yesu, binadamu Aliyaona haya na kila kitu Alichokiona kilimfanya kuhisi umuhimu na haja ya kazi Aliyokuwa Ameamua kuifanya wakati huu akiwa mwili. Hata ingawa Yeye Mwenyewe Alijua kwamba jukumu Alilohitaji kushughulikia Akiwa mwili lilikuwa kubwa mno, na namna ambavyo Angepitia maumivu ya kikatili, Alipomwona mwanadamu asiyejiweza ndani ya dhambi, Alipoona umaskini wa maisha yao na mapambano hafifu chini ya sheria, Alihuzunika zaidi na zaidi, na Akawa na hamu kubwa zaidi na zaidi ya kumwokoza binadamu kutoka dhambini. Haijalishi ni ugumu wa aina gani ambao Angepitia au ni aina gani ya maumivu Angehisi, Alikuwa akawa na ushupavu zaidi na zaidi katika kuwakomboa wanadamu, ambaye

alikuwa akiishi katika dhambi. Wakati wa mchakato huu, unaweza kusema kwamba Bwana Yesu alianza kuelewa waziwazi kazi Aliyohitajika kufanya na kile Alichokuwa Aameaminiwa kutekeleza. Alikuwa pia mwenye hamu kubwa zaidi ya kukamilisha kazi ambayo Alikuwa Aichukue—kushughulikia dhambi zote za mwanadamu, upatanisho wa Mungu na binadamu ili wasiishi tena katika dhambi naye Mungu Angeweza kusahau dhambi za binadamu kwa sababu ya sadaka ya dhambi, na hivyo basi kumruhusu kuendeleza kazi Yake ya kuwaokoa wanadamu. Yaweza kusemwa kwamba katika moyo wa Bwana Yesu, Alikuwa radhi kujitoa kwa ajili ya mwanadamu, kujitoa Mwenyewe. Alikuwa radhi pia kuchukua nafasi ya sadaka ya dhambi, kusulubishwa msalabani, na Alikuwa na hamu ya kukamilisha kazi hii. Alipoona hali za kusikitisha za maisha ya binadamu, Alitaka hata zaidi kukamilisha misheni Yake haraka iwezekanavyo, bila ya kuchelewa hata dakika au sekunde moja. Alipokuwa na hisia hii ya dharura, Alikuwa hafikirii namna ambavyo maumivu Yake binafsi yangukuwa wala hakufikiria kwa muda wowote zaidi kuhusu ni kiwango kipi cha udhalilishaji ambacho Angevumilia—Alishikilia azimio moja tu moyoni Mwake: Mradi tu Alijitoa Mwenyewe, mradi tu Angesulubishwa msalabani kama sadaka ya dhambi, mapenzi ya Mungu yangetendeka na Angeweza kuanza kazi mpya. Maisha ya wanadamu katika dhambi, hali yao ya kuwepo katika dhambi ingebadilika kabisa. Imani yake na kile Alichuamua kufanya vyote vilihusiana na kumwokoa binadamu, na Alikuwa na lengo moja tu: kufanya mapenzi ya Mungu ili Aweze kuanza kwa ufanisi hatua ambayo ingefuata katika kazi Yake. Haya ndiyo yaliyokuwa katika akili ya Bwana Yesu wakati huo.

Akiishi katika mwili, Mungu mwenye mwili Alimiliki ubinadamu wa kawaida; Alikuwa na hisia na kule kuwaza kwa mtu wa kawaida. Alijua furaha ilikuwa nini, maumivu yalikuwa nini na Alipowaona wanadamu katika hali hii ya maisha, Alihisi kwa kina kwamba kuwapatia watu kiasi cha mafunzo tu, kuwapatia kitu au kuwafunza kitu kusingewaongoza kutoka katika dhambi. Wala kuwafanya kutii amri pia kusingewakomboa kutoka katika dhambi—pale tu Alipozichukua dhambi za binadamu na kuwa mfano wa mwili wenye dhambi ndipo Alipoweza kuibadilisha na uhuru wa mwanadamu na kuibadilisha na msamaha wa Mungu kwa binadamu. Kwa hivyo baada ya Bwana Yesu kupitia na kushuhudia maisha ya binadamu katika dhambi, kulikuwa na tamanio kuu lililojionyesha katika moyo Wake—kuwaruhusu wanadamu kujiondoa kutoka katika maisha yao ya kupambana na dhambi. Tamanio hili lilimfanya kuhisi zaidi na zaidi kwamba lazima Aende katika msalaba na kuzichukua dhambi za binadamu haraka iwezekanavyo, kwa dharura. Hizi ndizo zilizokuwa fikira za Bwana Yesu wakati huo, baada ya Yeye kuishi na watu na kuwaona, kuwasikia, na kuhisi umaskini wa maisha yao ndani ya dhambi. Kwamba Mungu mwenye mwili Angekuwa na nia ya aina hii kwa mwanadamu, kwamba Angeweza kueleza na kufichua tabia ya aina hii—je, hili ni jambo ambalo mtu wa kawaida angekuwa nalo? Mtu wa

kawaida angeona nini akiishi katika mazingira ya aina hii? Angefikiria nini? Kama mtu wa kawaida angekumbwa na haya yote, angeangalia matatizo haya kwa mtazamo wa juu? Bila shaka hapana! Ingawa kuonekana kwa Mungu mwenye mwili ni kama mwanadamu, Anajifunza maarifa ya mwanadamu na kuongea lugha ya mwanadamu, na wakati mwingine Anaonyesha hata mawazo Yake kwa jinsi na hisia za mwanadamu, namna Anavyowaona wanadamu, kiini cha vitu, na namna ambavyo watu waliopotoka wanavyomwona mwanadamu na kiini cha vitu kwa hakika si sawa kabisa. Mtazamo Wake na kimo Anachosimamia ni jambo ambalo halifikiwi na mtu aliyepotoka. Hii ni kwa sababu Mungu ni ukweli, mwili Anaouvalia unamiliki pia kiini cha Mungu, na fikira Zake na kile ambacho kinadhihirishwa na ubinadamu Wake pia ni ukweli. Kwa watu waliopotoka, kile Anachoeleza katika mwili ni matoleo ya ukweli na maisha. Matoleo haya si ya mtu mmoja tu lakini kwa wanadamu wote. Kwa mtu yeyote aliyepotoka, katika moyo wake kunao tu wale watu wachache ambao wanahusiana na yeye. Kunao tu hao watu kadhaa ambao anawatunza ambao anajali kuwahusu. Wakati janga linakaribia, anafikiria kwanza kuhusu watoto wake binafsi, mume au mke au wazazi, na mtu mwenye moyo wa kujitoa zaidi kuhusu mwanadamu angefikiria zaidi kuhusu baadhi ya watu wa ukoo au rafiki mzuri; je yeye huwafikiria wengine? La hasha! Kwa sababu binadamu ni, kwa hakika, binadamu, na wanaweza tu kuangalia kila kitu kutoka kwa mtazamo na kutoka katika kimo cha mtu. Hata hivyo, Mungu mwenye mwili ni tofauti kabisa na mtu aliyepotoka. Bila kujali ni vipi ambavyo mwili wa Mungu mwenye mwili ulivyo wa kawaida, ulivyo kama wengine, ulivyo wa chini, au hata namna ambavyo watu wanamdharau Yeye, fikira Zake na mwelekeo Wake kwa wanadamu ni mambo ambayo hakuna binadamu angeweza kufuatisha na wala hakuna binadamu angeweza kuiga. Siku zote Atawaangalia wanadamu kutoka kwa mtazamo wa uungu, kutoka katika kimo cha madaraka Yake kama Muumba. Siku zote Atawaona wanadamu kupitia katika kiini na akili ya Mungu. Hawezi kabisa kuwaona wanadamu kutoka katika kimo cha mtu wa kawaida na kutoka kwa mtazamo wa mtu aliyepotoka. Watu wanapowaangalia wanadamu, wanawaangalia kwa mtazamo wa binadamu, na wanatumia mambo kama vile maarifa ya binadamu na masharti na nadharia za binadamu kama kipimo. Hali hii imo ndani ya mawanda ya kile ambacho watu wanaweza kuona kwa macho yao; ni ndani ya upana ambao watu waliopotoka wanaweza kutimiza. Mungu anapowatazama wanadamu, Anawatazama kwa macho ya kiungu, na Anatumia kiini Chake na kile Alichu nacho na kile Alichu kama kipimo. Mawanda haya yanajumuisha mambo ambayo watu hawawezi kuona, na hapo ndipo Mungu mwenye mwili na wanadamu waliopotoka walivyo tofauti kabisa. Tofauti hii inaamuliwa na viini tofauti vya wanadamu na vya Mungu na ndivyo vinavyoamua utambulisho na nafasi zao pamoja na mtazamo na kimo ambacho wanaona mambo. Je, unaona udhihirisho na ufichuzi wa Mungu Mwenyewe ndani ya Bwana Yesu? Unaweza kusema kwamba kile ambacho Bwana Yesu alifanya na kusema kilihusiana na huduma Yake na kazi ya usimamizi ya Mungu binafsi, kwamba yote hayo

yalikuwa ni udhihirisho na ufichuzi wa kiini cha Mungu. Ingawa Alikuwa na udhihirisho wa binadamu, kiini Chake cha kiungu na ufichuzi Wake wa kiungu hauwezi kukataliwa. Je, udhihirisho huu wa wanadamu ulikuwa udhihirisho wa kweli wa ubinadamu? Udhihirisho Wake wa ubinadamu ulikuwa, kwa kiini chake, tofauti kabisa na udhihirishaji wa ubinadamu wa watu waliopotoka. Bwana Yesu alikuwa Mungu mwenye mwili, na kama Angekuwa kweli mmojawapo wa wale wa kawaida, watu waliopotoka, Angeweza kuyaona maisha ya wanadamu ndani ya dhambi kutoka katika mtazamo wa kiungu? La hasha! Hii ndiyo tofauti kati ya Mwana wa Adamu na watu wa kawaida. Watu wote waliopotoka wanaishi ndani ya dhambi na wakati mtu yeyote anaiona dhambi, hana hisia zozote kuihusu hiyo dhambi; wako sawa tu, kama vile nguruwe anayeishi kwenye matope na hahisi chochote kamwe kuhusu kutokuwa na utulivu, au uchafu—anakula vizuri na kulala vizuri. Kama mtu anasafisha nyumba ya nguruwe, nguruwe kwa hakika hatahisi utulivu, na hatabakia akiwa msafi. Baada ya muda mfupi tu atakuwa tena akijigaragaza katika matope akiwa mtulivu kabisa, kwa sababu yeye ni kiumbe mchafu. Wakati binadamu wanapomwona nguruwe wanahisi kwamba anao uchafu na ukimsafisha yule nguruwe hahisi vyema zaidi—ndio maana hakuna anayemfuga nguruwe ndani ya nyumba yake. Namna ambavyo wanadamu wanavyomwona nguruwe itakuwa tofauti siku zote na namna ambavyo nguruwe wenyewe wanavyojihisi, kwa sababu wanadamu na nguruwe si wa aina moja. Na kwa sababu Mwana wa Adamu kwa mwili si wa aina moja na wanadamu waliopotoka, Mungu mwenye mwili tu ndiye Anayeweza kusimama kutoka kwa mtazamo wa kiungu, na kusimama kutoka katika kimo cha Mungu ili kuwaona wanadamu, ili kuona kila kitu.

Mungu anapokuwa mwili na kuishi miongoni mwa wanadamu, ni mateso yapi Anayopitia katika mwili? Yupo yeyote anayeelewa kwa kweli? Baadhi ya watu husema kwamba Mungu huteseka pakubwa, na ingawa Yeye ni Mungu Mwenyewe, watu hawaelewi kiini Chake na siku zote wanamchukulia Yeye kama mtu, hali ambayo humfanya Yeye kuhisi vibaya na kuona kwamba Amekosewa—wanasema kwamba mateso ya Mungu kwa kweli ni makubwa. Baadhi ya watu husema kwamba Mungu hana hatia na hana dhambi, lakini Yeye huteseka sawa na wanavyoteseka wanadamu, na Yeye hupitia mateso, matusi, na kuvunjiwa heshima pamoja na wanadamu; wanasema Yeye pia huvumilia kutoelewana na kutotiiwa na wafuasi Wake—kuteseka kwa Mungu kwa kweli hakuwezi kupimwa. Yamkini humwelewi Mungu kwa kweli. Kwa hakika, mateso haya unayoyaongelea hayaonekani kuwa mateso ya kweli kwake Mungu, kwa sababu kunayo mateso makubwa zaidi ya haya. Basi mateso ya kweli kwa Mungu Mwenyewe ni yapi? Mateso ya kweli ya mwili wa Mungu ni yapi? Kwa Mungu, wanadamu kutomwelewa Yeye haihesabiki kuwa ni mateso, na kwa watu kuwa kutokuwa na uelewano fulani wa Mungu na kwa kutomwona Yeye kama Mungu hakuhesabiki kuwa mateso. Hata hivyo, mara nyingi watu huhisi kwamba Mungu lazima alipitia dhuluma kubwa sana, kwamba

wakati Mungu yumo katika mwili Hawezi kuionyesha nafsi Yake kwa wanadamu na kuwaruhusu kuuona ukubwa Wake, na Mungu anajificha kwa unyenyekevu katika mwili duni na hivyo basi hali hii lazima ilikuwa ya kumpa Yeye maumivu makali. Watu hushikilia moyoni kile wanachoweza kuelewa na kile wanachoweza kuona kuhusu mateso ya Mungu, na kuweka aina zote za huruma kwake Mungu na mara nyingi hata wataisifia kidogo hali hiyo. Kwa uhakika, kunayo tofauti, kuna pengo kati ya kile watu wanachoelewa, kile watu wanachoelewa kuhusu mateso ya Mungu na kile Anachohisi kwa kweli. Nakwambia ukweli—kwa Mungu haijalishi kama ni Roho wa Mungu au mwili wa Mungu, mateso hayo si mateso ya kweli. Basi ni nini hasa ambacho kwa kweli Mungu huteseka? Hebu tuzungumze kuhusu mateso ya Mungu kutoka katika mtazamo wa Mungu mwenye mwili pekee.

Wakati Mungu anapokuwa mwili, kugeuka ndani wa wastani, mtu wa kawaida akiishi miongoni mwa wanadamu, miongoni mwa watu, je, Hawezi kuona na kuhisi mbinu za watu, sheria na falsafa zao za kuishi? Ni vipi ambavyo mbinu na sheria hizi zinamfanya Yeye kuhisi? Je, Anahisi kuwa na chuki katika moyo Wake? Kwa nini Ahisi chuki? Mbinu na sheria za kuishi za wanadamu ni gani? Zimekita mizizi katika kanuni gani? Ziko katika msingi upi? Mbinu, sheria, n.k za kuishi kwa wanadamu,—zote hizi zimeundwa kwa misingi ya mantiki, maarifa na falsafa ya Shetani. Wanadamu wanaoishi chini ya aina hizi za sheria hawana ubinadamu, hawana ukweli—wote wanaukataa ukweli, na ni wakatili kwa Mungu. Tunapoangalia kiini cha Mungu, tunaona kwamba kiini Chake ni kinyume kabisa na mantiki, maarifa na falsafa ya Shetani. Kiini Chake kimejaa haki, ukweli, na utakatifu na uhalisi mwingine wa mambo yote mazuri. Mungu, akimiliki kiini hiki na Akiishi miongoni mwa wanadamu—Anahisi vipi katika moyo Wake? Je, haujajaa maumivu? Moyo Wake umo katika maumivu, na maumivu haya ni kitu ambacho hakuna mtu anayeweza kuelewa wala kutambua. Kwa sababu kila kitu Anachokumbana nacho, kukabiliana nacho, kusikia, kuona na kupitia vyote ni upotovu wa wanadamu, uovu, na uasi wao dhidi ya, na upinzani wa ukweli. Kila kitu kinachotoka kwa wanadamu ndicho chanzo cha mateso Yake. Hivi ni kusema kwa sababu kiini Chake halisi si sawa na wanadamu waliopotoka, kupotoka kwa wanadamu kunakuwa ndiko chanzo cha mateso Yake makuu. Wakati Mungu anapokuwa mwili, Anaweza kupata mtu anayetumia lugha moja na Yeye? Hili haliwezi kupatikana miongoni mwa wanadamu. Hakuna anayeweza kupatikana anayeweza kuwasiliana, anayeweza kuwa na mabadilishano haya na Mungu—unaweza kusema Mungu anayo hisia aina gani? Yale mambo ambayo watu huzungumza ambayo wanapenda, ambayo wanafuatilia na kutamani yote yanahusu dhambi, na yana mielekeo ya uovu. Wakati Mungu anapokabiliana na haya, haya si kama kisu katika moyo Wake? Akiwa Amekabiliwa na mambo haya, Anaweza kuwa na furaha katika moyo Wake? Anaweza kupata kitulizo? Wale wanaoishi na Yeye ni wanadamu waliojaa uasi na uovu—je, moyo Wake utakosaje kuteseka? Mateso haya kwa kweli

ni makubwa vipi, na ni nani anayeyajali? Ni nani anayeyasikiliza? Na ni nani anayeweza kuyatambua? Watu hawana njia yoyote ya kuuelewa moyo wa Mungu. Mateso Yake ni kitu ambacho watu hawawezi hasa kutambua, na ubaridi, na kutojua kwa binadamu kunayafanya mateso ya Mungu kuwa yenye kina zaidi.

Kunao baadhi ya watu ambao huonea huruma hali ya Kristo kwa sababu kunao mstari katika Biblia unaosema: “Mbweha wana mashimo, na ndege wanavyo viota; lakini Mwana wa Adamu hana pahali pa kupumzisha kichwa chake.” Wakati watu wanaposikia haya, wanayatia moyoni na kuamini kwamba haya ndiyo mateso makubwa zaidi ambayo Mungu huvumilia, na mateso makubwa zaidi ambayo Kristo huvumilia. Sasa, tukiangalia katika mtazamo wa ukweli, hivyo ndivyo ilivyo? Mungu haamini kwamba ugumu huu ni mateso. Hajawahi kulia dhidi ya dhuluma hizi kwa ajili ya ugumu wa mwili, na hajawahi kuwalipizia kisasi wanadamu au Kujitoza na chochote. Hata hivyo, Anaposhuhudia kila kitu cha wanadamu, maisha yaliyopotoka na uovu wa wanadamu waliopotoka, Anaposhuhudia kwamba wanadamu wamo katika ung’amuzi wa Shetani na wamefungwa na Shetani na hawawezi kukwepa, kwamba wanaoishi ndani ya dhambi hawajui ukweli ni nini—Hawezi kuvumilia dhambi hizi zote. Chuki Yake kwa binadamu huongezeka siku baada ya siku, lakini lazima Avumilie yote haya. Haya ni mateso makuu ya Mungu. Mungu hawezi kujieleza kikamilifu hata sauti ya moyo Wake au hisia Zake miongoni mwa wafuasi Wake, na hakuna yeyote miongoni mwa wafuasi Wake anayeweza kuelewa kwa kweli mateso Yake. Hakuna yule ambaye hujaribu kuyaelewa au kuutuliza moyo Wake—moyo Wake huvumilia mateso haya siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, mara kwa mara. Unaona nini katika yote haya? Mungu hahitaji chochote kutoka kwa wanadamu kama malipo kwa kile Alichokitoa, lakini kwa sababu ya kiini cha Mungu, Hawezi kuvumilia kamwe uovu, upotovu na dhambi ya wanadamu, lakini Anahisi chukizo na chuki kupindukia, hali ambayo husababisha moyo wa Mungu na mwili Wake kuvumilia mateso yasiyoisha. Je, ungeyaona yote haya? Kuna uwezekano, hakuna yeyote kati yenu ambaye angeyaona kwa sababu hakuna yeyote kati yenu anayeweza kumwelewa Mungu kwa kweli. Baada ya muda mnaweza kuyapitia haya wenyewe kwa utaratibu.

Halafu, hebu tuangalie vifungu vifuatavyo katika maandiko.

9. Yesu Atenda Miujiza

1) Yesu Awalisha Watu Eelfu Tano

Yohana 6:8-13 Mmoja wa wanafunzi wake, Andrea, ndugu yake Simoni Petro, akasema kwake, Kuna mvulana hapa, aliye na mikate mitano ya shayiri nao samaki wawili wadogo: lakini ni yapi miongoni mwa watu wengi? Naye Yesu akasema, Wafanye watu waketi chini. Na

kulikuwa na nyasi nyingi pahali hapo. Kwa hivyo wanaume wakaketi chini, wakiwa idadi ya takribani elfu tano. Naye Yesu akaichukua ile mikate, na baada ya kutoa shukrani, akagawanya kwa wanafunzi, na wanafunzi wakawapa wale waliokuwa wameketi chini; na vivyo hivyo wale samaki kadiri kiasi walichotaka. Baada ya kushiba, alisema kwa wanafunzi wake, Ninyi kusanyeni vipande ambavyo vimebaki, ndiyo chochote kisipotezwe. Kwa hivyo walivikusanya pamoja, na wakavijaza vikapu kumi na mbili na vipande vya mikate mitano ya shayiri vilivyobaki baada ya wale watu kula.

2) Kufufuka kwa Lazaro Kwampa Mungu Utukufu

Yohana 11:43-44 Na baada ya yeye kuzungumza, akasema kwa sauti kuu, Lazaro, kuja nje. Na yeye ambaye alikuwa amefariki akatoka nje, akiwa amefungwa mkono na mguu na sanda: na uso wake ulikuwa umefungwa kwa kitambaa. Yesu akasema kwao, Mfungueni yeye, na mwache aondoke.

Kati ya miujiza iliyotendwa na Bwana Yesu, tumechagua tu hii miwili kwa sababu inatosha kuwaonyesha kile ambacho Ningependa kuzungumzia hapa. Miujiza hii miwili inashangaza ajabu, na inawakilisha hasa miujiza ya Bwana Yesu katika Enzi ya Neema.

Kwanza, hebu tuangalie ufahamu wa kwanza: Yesu Awalisha Watu Elfu Tano.

Dhana ya “mikate mitano na samaki wawili” ni ya aina gani? Ni watu wangapi ambao mikate mitano na samaki wawili hulisha kwa kawaida? Mkipima kulingana na hamu ya kula ya mtu wa kawaida, inaweza kutosha tu watu wawili. Hii ndiyo dhana ya kimsingi kabisa ya mikate mitano na samaki wawili. Hata hivyo, imeandikwa katika dondoo hii kwamba mikate mitano na samaki wawili viliwalisha watu wangapi? Imerekodiwa katika Maandiko hivi: “Na kulikuwa na nyasi nyingi pahali hapo. Kwa hivyo wanaume wakaketi chini, wakiwa idadi ya takribani elfu tano.” Tukilinganisha na mikate mitano na samaki wawili, elfu tano ni idadi kubwa? Ni nini maana ya idadi hii kuwa kubwa sana? Kutoka kwa mtazamo wa binadamu, kugawanya mikate mitano na samaki wawili kati ya watu elfu tano haitawezekana, kwa sababu tofauti kati ya idadi hizi ni kubwa mno. Hata kama kila mtu angepata tu kipande kidogo cha kutafuna, bado mikate hiyo isingetosha watu hao elfu tano. Lakini hapa Bwana Yesu alitenda muujiza—Hakuruhusu watu elfu tano kula hadi wakashiba tu, ila kulikuwa na vyakula vilivyobaki. Maandiko yanasema: “Baada ya kushiba, alisema kwa wanafunzi wake, Ninyi kusanyeni vipande ambavyo vimebaki, ndiyo chochote kisipotezwe. Kwa hivyo walivikusanya pamoja, na wakavijaza vikapu kumi na mbili na vipande vya mikate mitano ya shayiri vilivyobaki baada ya wale watu kula.” Muujiza huu uliwaruhusu watu kutambua utambulisho na hadhi ya Bwana Yesu, na uliwaruhusu pia kuona kwamba hakuna kisichowezezekana kwa Mungu—waliuona ukweli wa kudura ya

Mungu. Mikate mitano na samaki wawili viliweza kutosha kuwalisha watu elfu tano lakini kama kusingekuwa na chakula chochote, Mungu angeweza kuwalisha watu hao elfu tano? Bila shaka Angeweza! Huu ulikuwa muujiza, hivyo basi bila shaka watu walihisi hali hii kutoeleweka na wakahisi kwamba haikuaminika na iliwashangaza lakini kwa Mungu kufanya kitu kama hicho halikuwa kitu. Kwa sababu hili lilikuwa jambo la kawaida kwa Mungu, kwa nini litengwe ili liweze kufasiriwa? Kwa sababu kile kilichomo nyuma ya muujiza huu kimebeba mapenzi ya Bwana Yesu, ambayo hayajawahi kugunduliwa na wanadamu.

Kwanza, hebu tujaribu kuelewa watu hawa elfu tano walikuwa wa aina gani. Walikuwa wafuasi wa Bwana Yesu? Kutoka kwa Maandiko, tunajua kwamba hawakuwa wafuasi Wake. Walijua Bwana Yesu alikuwa nani? Bila shaka hawakujua! Kwa kiwango cha chini sana, hawakujua yule mtu aliyekuwa amesimama mbele yao alikuwa Kristo, au pengine baadhi ya watu walijua tu jina Lake lilikuwa nani, na kujua kitu kumhusu Yeye au walikuwa wamesikia kitu kuhusu mambo aliyokuwa Amefanya. Walikuwa na mshawasha tu kuhusu Bwana Yesu kutoka katika hadithi, lakini bila shaka hamwezi kusema kwamba wao walimfuata Yeye, wala hata Kumwelewa. Bwana Yesu alipowaona watu hawa elfu tano, walikuwa na njaa na Angefikiria tu kuwalisha hadi washibe, na hivyo basi ilikuwa katika muktadha huu ndipo Bwana Yesu aliporidhisha matamano yao. Baada ya kuyaridhisha matamano yao, ni nini kilichokuwa moyoni Mwake? Mwelekeo Wake kwa watu hawa waliotaka tu kula hadi kushiba ulikuwa upi? Wakati huu, fikira na mwelekeo Wake Bwana Yesu lazima ungehusu tabia ya Mungu na hali Yake halisi. Kuwa mbele ya watu hawa elfu tano waliokuwa na njaa na ambao walitaka tu kula chakula hadi kushiba, kuwa mbele ya watu hawa waliojaa mshawasha na matumaini kumhusu, Bwana Yesu alifikiria tu kutumia muujiza huu ili kuwatolea neema. Hata hivyo, Hakujipa tumaini sana kwamba watakuwa wafuasi Wake, kwani Alijua walitaka kujiunga na furaha hiyo na kuweza kula hadi kushiba, hivyo basi Aliweza kutumia kwa njia bora zaidi kile Alichokuwa nacho hapo, na Akatumia mikate mitano na samaki wawili kuwalisha watu elfu tano. Aliwafumbua macho watu hawa waliofurahia burudani hiyo, waliotaka kuiona miujiza, na wakaona kwa macho yao mambo yale ambayo Mungu mwenye mwili Angeweza kukamilisha. Ingawa Bwana Yesu alitumia kitu kinachoweza kushikika ili kuridhisha mshawasha wao, tayari Alijua katika moyo Wake kwamba watu hawa elfu tano walitaka tu kuwa na mlo mzuri, hivyo basi Hakusema chochote kamwe au kuwahubiria kamwe—Aliwaacha tu kuuona muujiza ukifanyika. Bila shaka Asingeweza kuwashughulikia watu hawa kwa njia sawa ambayo aliwashughulikia wanafunzi Wake ambao walimfuata Yeye kwa kweli, lakini katika moyo wa Mungu, viumbe vyote vilikuwa katika utawala Wake, na Angeviruhusu viumbe vyote katika macho Yake kufurahia neema ya Mungu kila ilipohitajika. Hata ingawa watu hawa hawakujua Yeye alikuwa nani au kumwelewa, au kuwa na picha yoyote fulani kumhusu au kutoa shukrani

Kwake hata baada ya kula mikate na samaki, hili halikuwa jambo ambalo Mungu Alijali kuhusu—Aliwapa watu hawa fursa nzuri ya kufurahia neema ya Mungu. Baadhi ya watu husema kwamba Mungu ana kanuni katika kile Anachofanya, na kwamba Hawaangalii wala kuwalinda wale wasioamini, na Yeye hasa hawaruhusu kufurahia neema Yake. Je, hivyo ndivyo ilivyo kwa hakika? Machoni mwa Mungu, mradi tu viwe ni viumbe vyenye uhai ambavyo Yeye Mwenyewe aliviumba, Ataweza kuvisimamia na kuvitunza; Atavitunza, Atavipangia, na Atavitawala katika njia tofauti. Hizi ndizo fikira na mtazamo wa Mungu kwa mambo yote.

Ingawa watu hawa elfu tano walioila mikate hiyo na samaki hawakupanga kumfuata Bwana Yesu, Hakuwa mkali kwao; baada ya wao kula hadi kushiba, je, mwajua kile Alichofanya Bwana Yesu? Je, Aliwahubiria chochote? Alienda wapi baada ya haya? Maandiko hayarekodi kwamba Bwana Yesu alisema chochote kwao; Alipokamilisha kutenda muujiza Wake Aliondoka kimya kimya. Hivyo basi Aliwawekea mahitaji yoyote watu hawa? Kulikuwa na chuki yoyote? Hakukuwepo na chochote kati ya hizi—Yeye hakutaka tu kutilia maanani akili yoyote kwa watu hawa ambao wasingeweza kumfuata, na kwa wakati huu moyo Wake ulikuwa katika maumivu. Kwa sababu alikuwa Ameuona upungufu wa wanadamu na Alikuwa amehisi namna ambavyo wanadamu walivyomkataa, na Alipowaona watu hawa au Alipokuwa na wao, upumbavu wa binadamu na kutojua kwao kulimfanya awe na huzuni sana na kukamwacha na maumivu katika moyo Wake, hivyo basi Alitaka tu kuwaacha watu hawa haraka iwezekanavyo. Bwana hakuwa na mahitaji yoyote kwao katika moyo Wake, Hakutaka kuwatilia maanani, Yeye hasa hakutaka kutumia nguvu Zake zozote kwao, na Alijua kwamba wasingeweza kumfuata—licha ya haya yote, mtazamo Wake kwao ulikuwa bado wazi kabisa. Alitaka tu kuwashughulikia kwa huruma, kuwarudishia neema—huu ndio uliokuwa mtazamo wa Mungu kwa kila kiumbe kilicho katika utawala Wake: kwa kila kiumbe, kishughulikie kwa huruma, watoshelezee mahitaji yao, wawaruzuku wao. Kwa sababu hasa ambayo Bwana Yesu alikuwa Mungu mwenye mwili, Aliweza kwa hali ya kimaumbile sana kufichua kiini cha Mungu binafsi na kuwashughulikia watu hawa kwa huruma. Aliwatendea kwa ukarimu na moyo wa rehema na uvumilivu. Haijalishi ni vipi watu hawa walimwona Bwana Yesu, na haikujalisha ni aina gani ya matokeo ambayo yangekuwepo, Alikitendea tu kila kiumbe kutokana na nafasi Yake kama Bwana wa uumbaji wote. Kile Alichofichua kilikuwa, bila kuachwa, tabia ya Mungu, na kile Alichochacho na kile Alichochacho. Kwa hivyo Bwana Yesu alifanya kitu kimya kimya, kisha Akaondoka kimya kimya—hii ni sura gani ya tabia ya Mungu? Unaweza kusema kwamba hii ni rehema ya upendo wa Mungu? Unaweza kusema kwamba Mungu ni Mwenye kujitolea? Mtu wa kawaida anaweza kufanya hivi? Bila shaka hawezi! Katika kiini, wale watu elfu tano ambao Bwana Yesu aliwalisha kwa mikate mitano na samaki wawili walikuwa kina nani? Tunaweza kusema kwamba walikuwa watu waliolingana na Yeye? Unaweza kusema kwamba wote walikuwa wakati kwa Mungu?

Inaweza kusemekana kwa uhakika kwamba hawakuwa kabisa wanaolingana na Bwana, na kiini chao halisi kilikuwa kikatili kabisa kwa Mungu. Lakini Mungu aliwashughulikia vipi? Alitumia mbinu ya kuutuliza ukatili wa watu kwa Mungu—mbinu hii inaitwa “huruma.” Yaani, ingawa Bwana Yesu aliwaona kama watendaji dhambi, machoni mwa Mungu walikuwa hata hivyo uumbaji Wake hivyo basi bado aliwashughulikia watendaji dhambi hawa kwa huruma. Huu ndio uvumilivu wa Mungu, na uvumilivu huu unaamuliwa na utambulisho na kiini cha Mungu binafsi. Hivyo basi, hili ni jambo ambalo hakuna mwanadamu aliyeumbwa na Mungu anaweza kufanya—Mungu pekee ndiye anayeweza kufanya hivi.

Unapoweza kutambua kwa kweli fikira na mtazamo wa Mungu kwa wanadamu, wakati unapoweza kuelewa kwa kweli hisia na kujali kwa Mungu kwa kila kiumbe, utaweza kuelewa kule kujitolea na upendo unaotumika kwa kila mmoja wa watu walioumbwa na Muumba. Haya yanapofanyika, utatumia maneno mawili kufafanua upendo wa Mungu—maneno hayo mawili ni yapi? Baadhi ya watu husema “mwenye kujitolea” na baadhi ya watu wakasema “kuwa na huruma nyingi ya kutoa msaada.” Kati ya kauli hizi mbili, “kuwa na huruma nyingi ya kutoa msaada” ndiyo kauli ambayo inafaa kwa kiasi kidogo zaidi kuufafanua upendo wa Mungu. Hii ni kauli ambayo watu hutumia kufafanua fikira na hisia za mtu kwa upana wa akili zake. Naichukia kweli kauli hii kwa sababu inarejelea ule utoaji wa msaada bila mpango na bila ubaguzi, bila kujali kanuni zozote. Ni maelezo ya kihisia za ziada za watu wajinga na waliochanganyikiwa. Wakati neno hili linatumika kufafanua upendo wa Mungu, bila shaka kuna nia ya kumaanisha kukufuru. Nina maneno mawili ambayo yanafafanua kwa usahihi zaidi upendo wa Mungu—maneno hayo mawili ni yapi? Neno la kwanza ni “kubwa.” Je, si neno hili huamsha na kuleta hisia? Neno la pili ni “pana.” Kunayo maana halisi katika maneno haya mawili mbili Ninazotumia katika kufafanua upendo wa Mungu. Kama yatachukuliwa kwa njia ya moja kwa moja, “kubwa” linafafanua ukubwa au wingi wa kitu, lakini haijalishi kitu hicho kina ukubwa gani—ni kitu ambacho watu wanaweza kugusa na kuona. Hii ni kwa sababu kipo, si kifaa cha kidhahania na kinapatia watu hisia kwamba kwa kiasi fulani kina usahihi na hali ya kimatendo. Haijalishi kama unakiangalia kutoka katika mtazamo bapa au wa pande zote tatu; huhitajiki kufikiria uwepo wake, kwa sababu ni kitu ambacho kwa kweli kipo. Hata ingawa kwa kutumia “kubwa sana” kufafanua upendo wa Mungu kunaweza kuhisiwa kana kwamba tunataka kupima wingi wa upendo Wake, lakini hata hivyo linatoa hisia kwamba hauwezi kupimwa. Nasema kwamba upendo wa Mungu unaweza kupimwa kwa sababu upendo Wake si aina fulani ya kitu kisichojulikana, wala hauchipuki tu kutoka kwa ngano yoyote. Badala yake, ni kitu cha kutumiwa kwa pamoja na vitu vyote katika utawala wa Mungu, na ni kitu cha kufurahiwa na viumbe vyote hadi kwa viwango tofauti na kutoka katika mitazamo tofauti. Ingawa watu hawawezi kukiona au kukigusa, upendo huu huleta maendelezo na maisha katika vitu vyote

kwani kinafichuliwa hatua kwa hatua katika maisha yao, na wanahesabu na kushuhudia upendo wa Mungu wanaofurahia kila wakati. Nasema kwamba upendo wa Mungu hauwezi kuhesabiwa kwa sababu fumbo la Mungu la Yeye kukidhi na kuimarisha vitu vyote ni kitu ambacho ni kigumu kwa wanadamu kuelewa, kama vile tu zilivyo fikira za Mungu katika vitu vyote na hasa vile vya mwanadamu. Hivyo ni kusema hakuna anayejua damu na machozi ambayo Muumba ametoa kwa sababu ya wanadamu. Hakuna anayeweza kufahamu, hakuna anayeweza kuelewa kina au uzito wa upendo ambao Muumba anao kwa ajili ya wanadamu, aliowaumba kwa mikono Yake binafsi. Kufafanua upendo wa Mungu kama mkubwa sana ni kuwasaidia watu kutambua na kuelewa upana wake na ukweli wa uwepo wake. Iko hivyo ili watu waweze kufahamu kwa kina zaidi maana halisi ya neno “Muumba,” na ili watu waweze kupata ufahamu wa kina zaidi wa maana ya “uumbaji.” Neno “pana” kwa kawaida huwa linafafanua nini? Linatumika kwa ujumla kumaanisha bahari au ulimwengu kama vile ulimwengu mpana au bahari pana. Ule mtanuko na kina kitulivu cha ulimwengu unazidi ufahamu wa binadamu na ni kitu ambacho kinanata fikra za binadamu, ambacho kwacho wamejawa na upendezwaji. Fumbo lake na umuhimu wake vyote vimo katika uwezo wa kuonekana lakini haviwezi kufikika. Unapofikiria kuhusu bahari, unafikiria kuhusu upana wake—yaonekana isiyo na mipaka, na unaweza kuhisi ile hali ya bahari hiyo kuwa fumbo na ujumuishwaji wake pia. Ndiyo maana Nimetumia neno “pana” kufafanua upendo wa Mungu. Ni kuwasaidia watu wahisi namna neno hilo lilivyo na thamani, na ili wahisi ule urembo wa kipekee wa upendo Wake, na kwamba nguvu za upendo wa Mungu haziishi na zimeenea. Ni kwa minajili ya kuwasaidia kuhisi utakatifu wa upendo Wake, na heshima pamoja na hali ya kutoweza kukosewa ya Mungu ambayo inafichuliwa kupitia upendo Wake. Sasa unafikiri kwamba “pana” ni neno linalofaa kufafanua upendo wa Mungu? Je, upendo wa Mungu unaweza kufikia maana ya maneno haya mawili, “kubwa sana” na “pana”? Bila shaka! Katika lugha ya binadamu, maneno haya mawili tu ndiyo ambayo yanafaa kwa kiasi fulani, na kwa kiasi fulani yanakaribia kuufafanua upendo wa Mungu. Je, huoni hivyo? Kama Ningewaulizeni kuufafanua upendo wa Mungu, je, mngatumia kauli hizi mbili? Kuna uwezekano mkubwa zaidi, msingeyatumia kwa sababu ufahamu na utambuzi wenu wa upendo wa Mungu ni finyu na unafikia tu mtazamo bapa, na bado haujakwea ngazi hadi katika ule urefu wa nafasi ya pande zote tatu. Hivyo basi kama Ningetaka mfafanue upendo wa Mungu, mngehisi kwamba mnakosa maneno; huenda pengine hata mtakosa kuongea kabisa. Maneno haya mawili ambayo Nimeyazungumzia leo yanaweza kuwa magumu kwako kuelewa, au pengine kwa ufupi tu hukubali. Hali hii inaweza kuongelea tu hoja kwamba utambuzi na ufahamu wako wa upendo wa Mungu ni wa juujuu na ndani ya upana mwembamba. Nimesema awali kwamba Mungu ni mwenye kujitolea—unakumbuka neno kujitolea? Inaweza kusemekana kwamba upendo wa Mungu unaweza kufafanuliwa tu kuwa wa kujitolea? Je, si haya si mawanda membamba mno? Mnafaa kutafakari suala hili zaidi ili kuweza kufaidika kutoka kwalo.

Yale yaliyotajwa hapo juu ndiyo yale tuliyoona ya tabia ya Mungu na kiini Chake kutoka katika muujiza wa kwanza. Hata ingawa ni hadithi ambayo watu wameisoma kwa maelfu kadhaa ya miaka, inao mtiririko mwepesi, na inaruhusu watu kuweza kuona suala la pekee, ilhali katika mtiririko huu mwepesi tunaweza kuona kitu chenye thamani zaidi, hali ambayo ni tabia ya Mungu na kile Alichacho na kile Alichacho. Mambo haya kuwa Alichacho na kile Alichacho yanamwakilisha Mungu Mwenyewe, na ni maelezo ya fikira za Mungu binafsi. Wakati Mungu anapoonyesha fikira Zake, ni udhihirisho wa sauti ya moyo Wake. Anatumai kwamba kutakuwa na watu wanaoweza kumwelewa Yeye, kumjua Yeye na wanafahamu mapenzi Yake, na Anatumai kutakuwa na watu wanaoweza kuisikia sauti ya moyo Wake na wataweza kushirikiana kwa bidii ili kuridhisha mapenzi Yake. Na vitu hivi ambavyo Bwana Yesu alifanya vilikuwa ni maelezo ya kimya ya Mungu.

Halafu, hebu tuangalie dondoo hii: Kufufuka kwa Lazaro Kwatukuza Mungu.

Mnayo picha gani baada ya kusoma dondoo hii? Umuhimu wa muujiza huu ambao Bwana Yesu alitenda ulikuwa mkubwa zaidi kuliko ule wa awali kwa sababu hakuna muujiza ambao unajitokeza zaidi kuliko ule wa kufufua binadamu aliyekufa na kutoka katika kaburi. Bwana Yesu kufanya kitu kama hiki kulikuwa na umuhimu mkubwa mno katika enzi hiyo. Kwa sababu Mungu alikuwa mwili, watu waliweza kuona tu kuonekana Kwake kwa kimwili, upande Wake wa kimatendo, na upande Wake usio na umuhimu. Hata kama baadhi ya watu waliona na kuelewa hulka Yake fulani au nguvu Zake ambazo alionekana kuwa nazo, hakuna aliyejua pale ambapo Bwana Yesu alipotokea, ambaye kiini Chake cha kweli kilikuwa, na nini kingine zaidi ambacho Angeweza kufanya. Haya yote hayakujulikana kwa mwanadamu. Watu wengi mno walitaka ithibati ya kitu hiki, na kuujuu ukweli. Je, Mungu angeweza kufanya kitu ili kuthibitisha utambulisho Wake Mwenyewe? Kwa Mungu, huu ulikuwa upepo mwanana—lilikuwa jambo rahisi sana. Angefanya kitu popote, wakati wowote ili kuthibitisha utambulisho na kiini Chake, lakini Mungu alikuwa na njia Yake ya kufanya mambo—kwa mpango, na kwa hatua. Hakufanya vitu bila mpangilio; Alitafuta muda unaofaa, na fursa inayofaa kufanya kitu chenye maana zaidi kwa wanadamu kuweza kuona. Hili lilithibitisha mamlaka Yake na utambulisho Wake. Hivyo basi, kufufuka kwa Lazaro kungeza kuthibitisha utambulisho wa Bwana Yesu? Hebu tuangalie kifungu hiki cha maandiko: “Na baada ya yeye kuzungumza, akasema kwa sauti kuu, Lazaro, kuja nje. Na yeye ambaye alikuwa amefariki akatoka nje...” Wakati Bwana Yesu alipofanya haya, Alisema tu jambo moja: “Lazaro, kuja nje.” Kisha Lazaro akatoka nje ya kaburi—hii ilikamilika kwa sababu ya mstari mmoja uliotamkwa na Bwana. Katika wakati huu, Bwana Yesu hakuweza kuandaa madhabahu, na Hakutekeleza hatua zote nyingine. Alisema tu jambo moja. Hili linaweza kutaitwa muujiza au amri? Au lilikuwa aina fulani wa uchawi? Kwa juujuu, yaonekana ingeweza kuitwa muujiza, na ukiangalia hali hiyo kutoka mtazamo wa kisasa,

bila shaka mnaweza bado kuliita muujiza. Hata hivyo, bila shaka hali hiyo isingeweza kuitwa apizo la kuiita nafsi kurudi kutoka kwa wafu, na bila shaka si uchawi. Ni sahihi kusema kwamba muujiza huu ulikuwa ni onyesho la kawaida zaidi, dogo ajabu la mamlaka ya Muumba. Haya ndiyo mamlaka, na uwezo wa Mungu. Mungu ana mamlaka ya kumwacha mtu afe, kuruhusu nafsi yake iondoke mwilini mwake na kurudi kuzimu au popote pale itakapoenda. Mtu anapokufa, na anakokwenda baada ya kifo—haya yanaamuliwa na Mungu. Yeye anaweza kufanya haya wakati wowote na mahali popote. Yeye hazuiliwi na binadamu, matukio, vifaa, nafasi au mahali. Akitaka kulifanya Anaweza kulifanya, kwa sababu vitu vyote na viumbe vyenye uhai vinatawaliwa na Yeye, na vitu vyote vinaongezeka, vinaishi na kuangamia kwa neno Lake na mamlaka Yake. Anaweza kumfufua binadamu aliyekufa, na pia hiki ni kitu Anachoweza kufanya wakati wowote mahali popote. Haya ndiyo mamlaka ambayo Muumbaji pekee humiliki.

Bwana Yesu alipofanya kitu kama vile kumleta Lazaro kutoka kwa wafu, lengo Lake lilikuwa ni kutoa ithibati kwa wanadamu na Shetani aweze kuona, na kuacha wanadamu na Shetani kujua kwamba kila kitu cha wanadamu, maisha na kifo cha wanadamu vyote vinaamuliwa na Mungu, na kwamba ingawa Alikuwa amekuwa mwili ilivyo kama siku zote, Alibaki katika mamlaka juu ya ulimwengu wa kimwili unaoweza kuonekana pamoja na ulimwengu wa kiroho ambao wanadamu hawawezi kuuona. Huku kulikuwa kuwaruhusu wanadamu na Shetani kujua kwamba kila kitu cha wanadamu hakiko katika amri ya Shetani. Huu ulikuwa ni ufunuo na onyesho la mamlaka ya Mungu, na ilikuwa pia njia ya Mungu kuutuma ujumbe wake kwa viumbe vyote kwamba maisha na kifo cha wanadamu kimo mikononi mwa Mungu. Bwana Yesu kumfufua Lazaro—kutenda kwa aina hii ni mojawapo ya njia za Muumba za kumfunza na kumwelekeza wanadamu. Ilikuwa ni hatua thabiti ambapo Aliutumia uwezo Wake na mamlaka Yake kuwaelekeza wanadamu, na kuwatolea wanadamu. Ilikuwa njia bila matumizi ya maneno kwa Muumba ya kuwaruhusu wanadamu kuweza kuuona ukweli wa Yeye kuwa na mamlaka juu ya viumbe vyote. Ilikuwa njia Yake ya kuwaambia binadamu kupitia kwa hatua za kimatendo kwamba hamna wokovu mbali na kupitia Yeye. Mbinu za aina hii za kimya za Yeye kuwaelekeza wanadamu zinadumu milele—hazifutiki, na iliweza kuleta katika mioyo ya wanadamu mshtuko na kupatikana kwa nuru ambayo haiwezi kufifia. Kufufuliwa kwa Lazaro kulimtukuza Mungu—hali hii inayo athari ya kina katika kila mojawapo wa wafuasi wa Mungu. Inakita mizizi kwa kila mmoja anayeelewa kwa kina tukio hili, ufahamu, maono kwamba ni Mungu tu anayeweza kuamuru maisha na kifo cha wanadamu. Ingawa Mungu ana aina hii ya mamlaka, na ingawa Aliutuma ujumbe kuhusu uhuru Wake dhidi ya maisha na kifo cha wanadamu kupitia kwa kufufuka kwa Lazaro, hii haikuwa kazi Yake ya msingi. Mungu katu hafanyi kitu bila maana. Kila kitu Anachofanya kina thamani kuu na kito

kupita ndani ya ghala la hazina. Bila shaka Yeye hangefanya “kuwa na mtu kutoka katika kaburi lake” kuwa sababu ya kimsingi au lengo au sababu kuu katika kazi Yake. Mungu hafanyi chochote ambacho hakina maana. Kufufuka kumoya kwa Lazaro kunatosha kuonyesha mamlaka ya Mungu. Kunatosha kuthibitisha utambulisho wa Bwana Yesu. Hii ndiyo sababu Bwana Yesu hakurudia aina hii ya muujiza. Mungu hufanya mambo kulingana na kanuni Zake binafsi. Katika lugha ya binadamu, ingekuwa kwamba Mungu anajali kazi muhimu. Yaani, wakati Mungu anapofanya mambo Hapotoki kutoka kwenye kusudio Lake la kazi. Anajua ni kazi gani Anayotaka kutekeleza katika awamu hii, kile Anachotaka kukamilisha, na Atafanya kazi mahususi kulingana na mpango Wake. Kama mtu aliyepotoka angekuwa na aina hiyo ya uwezo, angekuwa akifikiria tu kuhusu njia za kufichua uwezo wake ili wengine wajue namna alivyokuwa thabiti, hivyo basi kumwinamia, ili aweze kuwadhibiti na kuwameza. Huu ndio uovu unaotoka kwa Shetani—huu unaitwa upotovu. Mungu hana tabia kama hiyo, na Hana kiini kama hicho. Kusudio Lake katika kufanya mambo si kujionyesha Mwenyewe, lakini kuwapa wanadamu ufunuo na mwongozo zaidi, ili watu waweze kuona mifano michache katika Biblia kuhusu aina hii ya jambo. Hii haimaanishi kwamba uwezo wa Bwana Yesu ulikuwa finyu, au kwamba asingeweza kufanya jambo la aina hiyo. Ni kwamba Mungu hakutaka tu kulifanya jambo hilo, kwa sababu Bwana Yesu kumfufua Lazaro kulikuwa na umuhimu wa kimatendo kabisa, na pia kwa sababu kazi kuu ya Mungu kuwa mwili haikuwa ni kutenda miujiza, haikuwa ni kuwaleta watu kutoka katika kifo, lakini ilikuwa ni kazi ya ukombozi wa wanadamu. Hivyo basi, wingi wa kazi ambayo Bwana Yesu alikamilisha ilikuwa ni kuwafunza watu, kuwatoshelezea haja zao, na kuwasaidia, na mambo kama vile kumfufua Lazaro yalikuwa tu mambo madogo ya huduma ambayo Bwana Yesu alitekeleza. Hata zaidi, mnaweza kusema kwamba “kujionyesha” si sehemu ya kiini cha Mungu, hivyo basi kutoonyesha miujiza zaidi hakukuwa kujizuia kimakusudi, wala hakukuwa kwa sababu ya vizuizi vya kimazingira, na bila shaka hakukuwa kwa sababu ya ukosefu wa uwezo.

Bwana Yesu alipomleta Lazaro kutoka kwa wafu, Alitumia mstari mmoja: “Lazaro, kuja nje.” Hakusema kitu kingine mbali na hiki—maneno haya yanawakilisha nini? Yanawakilisha hoja kwamba Mungu anaweza kukamilisha chochote kupitia maongezi, kukiwemo kumfufua mtu aliyekufa. Mungu alipoumba viumbe vyote, Alipoumba ulimwengu, Alifanya hivyo kwa maneno—amri za kutamkwa, maneno yaliyotamkwa kwa mamlaka, na hivyo tu viumbe vyote viliumbwa. Yalikamilishwa hivyo. Mstari huu mmoja uliozungumzwa na Bwana Yesu ulikuwa sawa na maneno yaliyotamkwa na Mungu alipoziumba mbingu na dunia na viumbe vyote; mstari huo pia uliweza kushikilia mamlaka ya Mungu, uwezo wa Muumba. Viumbe vyote viliumbwa na vikasimama kwa sababu ya matamshi kutoka kwa kinywa cha Mungu, na vivyo hivyo, Lazaro alitembea kutoka katika kaburi lake kwa sababu ya matamshi kutoka katika kinywa cha Bwana

Yesu. Haya ndiyo yaliyokuwa mamlaka ya Mungu, yaliyoonyeshwa na kutambuliwa katika mwili Wake. Aina hii ya mamlaka na uwezo vilimilikiwa na Muumba, na kwa Mwana wa Adamu ambaye kwake Muumba alitambuliwa. Huu ndio ufahamu uliofunzwa kwa mwanadamu kwa Mungu kumleta Lazaro kutoka kwa wafu. Hayo ndiyo yote katika mada hii. Halafu, hebu tuyasome maandiko.

10. Hukumu ya Mafarisayo kwa Yesu

Marko 3:21-22 Na wakati marafiki zake walisikia kuhusu hilo, walitoka kumshika: kwani walisema, Yeye si wa akili sawa. Nao waandishi waliokuja kutoka Yerusalemu walisema, Ana Beelzebubi, na kupitia mwana wa mfalme wa mapepo huwaondoa mapepo.

11. Mafarisayo Kukemewa na Yesu

Mat 12:31-32 Ndiyo sababu nawaambieni, Wanadamu watasamehewa kila namna ya dhambi na kukufuru: lakini wanadamu hawatasamehewa kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu. Na yeyote ambaye atasema neno dhidi ya Mwana wa Adamu atasamehewa: ila yeyote ambaye atasema dhidi ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa, wala katika dunia hii, wala katika dunia itakayokuja.

Mat 23:13-15 Lakini ole wenu nyinyi, waandishi na Mafarisayo, mlio wanafiki! Kwa maana mnafunga ufalme wa mbinguni wasiingie wanadamu: kwani ninyi hamwingii wenyewe, wala hamkubali wanaoingia ndani waingie. Ole wenu nyinyi, waandishi na Mafarisayo, mlio wanafiki! Kwani mnazila nyumba za wanawake wajane, na mnatoa sala ndefu kwa kujifanya: kwa hivyo mtapokea laana kubwa zaidi. Ole wenu nyinyi, waandishi na Mafarisayo, mlio wanafiki! Kwa maana mnazingira bahari na ardhi kwa ajili ya kumfanya mtu kubadili imani, na anapobadili, mnamfanya awe mwana wa kuzimu mara dufu zaidi kuwaliko.

Kunazo dondoo mbili tofauti hapo juu—hebu kwanza tuangalie dondoo ya kwanza: Hukumu ya Mafarisayo kwa Yesu.

Katika Biblia, tathmini ya Mafarisayo kwa Yesu Mwenyewe na mambo alioyafanya ilikuwa: “walisema, Yeye si wa akili sawa. ... Ana Beelzebubi, na kupitia mwana wa mfalme wa mapepo huwaondoa mapepo” (Marko 3:21-22). Hukumu ya waandishi na Mafarisayo kwa Bwana Yesu haikuwa ikiiga mambo au ikifikiria tu kutoka popote—ilikuwa hitimisho yao kuhusu Bwana Yesu kutokana na yale walioyaona na kuyasikia kuhusu vitendo Vyake. Ingawa hitimisho yao ilitolewa kwa njia isiyo ya kweli au ya uongo kwa jina la haki, na kuonekana mbele ya watu ni kana kwamba ilikuwa imeshughulikiwa vyema, kiburi ambacho walitumia kumhukumu Bwana Yesu kilikuwa kigumu hata kwa wao wenyewe kuvumilia. Nguvu zao

mchafukoge za chuki yao kwa Bwana Yesu ziliweza kufichua maono yao binafsi yasiyo na mipaka na sura zao za kishetani na uovu, pamoja na maumbile yao yenye nia mbaya ya kumpinga Mungu. Mambo haya waliyoyasema katika hukumu yao kwa Bwana Yesu yaliendeshwa na maono yao yasiyo na misingi, ya wivu, na hali ya ubovu na ubaya na ukatili wao dhidi ya Mungu na ukweli. Hawakuchunguza chanzo cha hatua za Bwana Yesu wala kuchunguza kiini cha kile Alichosema au kufanya. Badala yake, walimshambulia bila mpango, bila subira, kwa njia za kishenzi, na kwa makusudi ya kijicho pamoja na kutupilia mbali kile Alichokuwa Amefanya. Hii ilikuwa hadi kufikia kiwango cha kutupilia mbali Roho Wake bila kubagua, Yaani, Roho Mtakatifu, Roho wa Mungu. Hivi ndivyo waliyomaanisha waliposema “Amerukwa na akili,” “Beelzebuli,” na “mkuu wa pepo.” Hii ni kusema kwamba walisema Roho wa Mungu alikuwa Beelzebuli na pia mkuu wa pepo. Waliweza kupatia sifa ya kazi ambayo Roho wa Mungu mwenye mwili alikuwa amevalia kama kurukwa akili. Hawakukufuru tu Roho wa Mungu kama Beelzebuli na mkuu wa pepo, lakini waliishutumu kazi ya Mungu. Walimshutumu na kumkufuru Bwana Yesu Kristo. Kiini cha upingaji wao na kukufuru Mungu kilikuwa sawa kabisa na kiini cha Shetani na upingaji wa Shetani na kumkufuru Mungu. Wao hawakuwakilisha wanadamu waliopotoka tu, lakini hata zaidi walikuwa mfano halisi wa Shetani. Walikuwa ni njia ya Shetani kutumia miongoni mwa wanadamu, na walikuwa washiriki na watumishi wa Shetani. Kiini cha kukufuru kwao na utovu wao wa nidhamu kwa Bwana Yesu Kristo ndicho kilichokuwa mapambano yao na Mungu kwa ajili ya hadhi, mashindano yao na Mungu, na mapambano yao na Mungu yasiyoisha. Kiini cha upingaji wao kwa Mungu na mwelekeo wao wa ukatili kwake Yeye, pamoja na maneno yao na fikira zao moja kwa moja vilimkufuru na kumghadhabisha Roho wa Mungu. Hivyo basi, Mungu aliamua hukumu inayofaa ya na yale waliyoyasema na kufanya, na akaamua matendo yao kuwa dhambi ya kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu. Dhambi hii haiwezi kusameheka ulimwenguni humu na hata ulimwengu unaokuja, kama vile tu maandiko yafuatayo yanasema: “Wanadamu hawatasamehewa kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu” na “Yeyote ambaye atasema dhidi ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa, wala katika dunia hii, wala katika dunia itakayokuja.” Leo, hebu tuzungumzie maana halisi ya maneno haya kutoka kwa Mungu “hatasamehewa, wala katika dunia hii, wala katika dunia itakayokuja.” Hii ni, acha tuweke wazi namna ambavyo Mungu hukamilisha matamshi yake: “haitasamehewa, wala katika dunia hii, wala katika dunia itakayokuja.”

Kila kitu ambacho tumezungumzia kuhusu yote haya kinahusiana na tabia ya Mungu, na mweleko Wake kwa watu, masuala na mambo, na mambo. Kikawaida, dondoo hizo mbili hapo juu haziwezi kuachwa. Je, mlitambua chochote katika dondoo hizi mbili za maandiko? Baadhi ya watu husema wanaiona ghadhabu ya Mungu. Baadhi ya watu husema wanauona upande wa tabia ya Mungu ambao hauvumilii kosa la wanadamu, na kwamba watu wakifanya kitu ambacho

kinamkufuru Mungu, hawatapata msamaha Wake. Licha ya ukweli kwamba watu wanaona na kutambua ghadhabu na kutovumilia makosa ya wanadamu kwa Mungu katika vifungu hivi viwili, bado hawaelewi kwa kweli mtazamo Wake. Dondoo hizi mbili zinao ufafanuzi wa mwelekeo na mtazamo wa kweli wa Mungu kwa wale wanaomkufuru na kumghadhabisha Yeye. Dondoo hii katika maandiko inashikilia maana halisi ya mwelekeo na mtazamo Wake: “Yeyote ambaye atasema dhidi ya Roho Mtakatifu, hatasamehewa, wala katika dunia hii, wala katika dunia itakayokuja.” Watu wanapomkufuru Mungu, wakati wanapomghadhabisha Yeye, Yeye hutoa hukumu, na hukumu hii ndiyo matokeo yaliyotolewa na Yeye. Hali hii inafafanuliwa hivi katika Biblia: “Ndiyo sababu nawaambieni, Wanadamu watasamehewa kila namna ya dhambi na kukufuru: lakini wanadamu hawatasamehewa kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu” (Mat 12:31), na “Lakini ole wenu nyinyi, waandishi na Mafarisayo, mlio wanafiki!” (Mat 23:13). Hata hivyo, imerekodiwa katika Biblia matokeo yapi yalikuwepo kwa wale waandishi na Mafarisayo, pamoja na wale watu waliosema Alikuwa amerukwa na akili baada ya Bwana Yesu kuyasema mambo hayo? Je, imerekodiwa kama walipata adhabu yoyote? Kuna uhakika kwamba hakukuwa na adhabu: Kusema hapa kwamba “hakukuwa” si kwamba haikurekodiwa, lakini kwa hakika hakukuwa na matokeo yoyote ambayo yangeonekana kwa macho ya binadamu. Neno hili “hakukuwa” linaelezea suala, yaani, mwelekeo na kanuni za Mungu katika kushughulikia mambo fulani. Namna ambavyo Mungu anawatendea watu wanaomkufuru au hata wanaompinga, au hata wale wanaomkashifu—watu wanaomshambulia kimakusudi, kumkashifu, na kumlaani—hajifanyi kwamba kila kitu kiko sawa. Anao mwelekeo wazi kwa hawa. Anawadharau watu hawa, na moyoni Mwake anawashutumu. Anatangaza waziwazi hata matokeo kwa ajili yao, ili watu waweze kujua kwamba Anao mwelekeo wazi kwao wanaomkufuru Yeye, na ili wajue namna atakavyoamua matokeo yao. Hata hivyo, baada ya Mungu kusema mambo haya, watu bado wangeona kwa nadra ukweli wa namna ambavyo Mungu angeshughulikia watu hao, na wasingeelewa kanuni zinazotawala matokeo ya Mungu, hukumu Yake kwao. Hiyo ni kusema, wanadamu hawawezi kuuona mwelekeo na mbinu fulani za Mungu katika kuwashughulikia. Hali hii inahusu kanuni za Mungu za kufanya mambo. Mungu hutumia ujio wa hoja katika kushughulikia tabia yenye uovu ya baadhi ya watu. Yaani, Hatangazi dhambi yao na haamui matokeo yao, lakini Anatumia moja kwa moja ujio wa hoja ili kuwaruhusu kuadhibiwa, wao kupata adhabu wanayostahili. Wakati hoja hizi zinapofanyika, ni miili ya watu inayoteseka kwa adhabu; hili ni jambo ambalo linaweza kuonekana kwa macho ya binadamu. Wakati wa kushughulikia tabia ya uovu kwa baadhi ya watu, Mungu huwalaani tu kwa matamshi, lakini wakati uo huo, ghadhabu ya Mungu huwapata, na adhabu wanayopokea inaweza kuwa jambo ambalo watu hawalioni, lakini aina hii ya matokeo inaweza kuwa hata mbaya zaidi kuliko matokeo ambayo watu wanaweza kuona ya kuadhibiwa au kuuawa. Hii ni kwa sababu katika hali zile ambazo Mungu ameamua kutomwokoia mtu wa aina hii, kutoonyesha

tena rehema au uvumilivu kwao, kutowapa fursa zaidi, mwelekeo Anaouchukua kwao ni kuwaweka pembeni. Ni nini maana ya “kuweka pembeni”? Maana ya kauli hii kibinafsi ni kuweka kitu kwa upande mmoja, kutokizingatia tena. Lakini hapa, wakati Mungu “anapomweka mtu pembeni,” kuna fafanuzi mbili tofauti kuhusu kile Alichu: Ufafanuzi wa kwanza ni kwamba Amempa Shetani kuyashughulikia maisha ya mtu huyo, na kila kitu cha mtu huyo. Mungu hatamwajibikia tena na Hataweza kumsimamia tena. Kama mtu huyo amerukwa na akili, au ni mpumbavu, na kama katika maisha au kifo, au kama angeshushwa jahanamu ili kupata adhabu yake, hayo yote yasingemhusu Mungu. Hiyo ingemaanisha kwamba kiumbe hicho hakitakuwa na uhusiano wowote na Muumba. Ufafanuzi wa pili ni kwamba Mungu ameamua kwamba Yeye Mwenyewe anataka kufanya kitu na mtu huyu, kwa mikono Yake mwenyewe. Inawezekana kwamba Ataweza kutumia huduma ya mtu wa aina hii, au kwamba atatumia mtu wa aina hii kama foili^[b]. Inawezekana kwamba Atakuwa na njia maalum ya kushughulikia mtu wa aina hii, njia maalum ya kumshughulikia—kama tu Paulo. Hii ndio kanuni na mwelekeo katika moyo wa Mungu kuhusu namna Alivyoamua kumshughulikia mtu wa aina hii. Hivyo basi wakati watu wanapompinga Mungu, na kumkashifu na kumkufuru Yeye, kama wataendelea kusema ubaya kuhusu tabia Yake, au kama watafikia ile hali ya kimsingi ya Mungu, athari zake hazifikiriki. Athari zile mbaya zaidi ni kwamba Mungu anayakabidhi maisha yao na kila kitu chao kwa Shetani, mara moja na kabisa. Hawatasamehewa daima dawamu. Hii inamaanisha kwamba mtu huyu amekuwa chakula katika kinywa cha Shetani, mwanasesere katika mikono yake, na kuanzia hapo, Mungu hahusiki naye. Mnaweza kufikiria ni aina gani ya masikitiko iliyokuweco wakati Shetani alipomjaribu Ayubu? Katika hali kwamba Shetani hakuruhusiwa kuyadhuru maisha ya Ayubu, Ayubu aliteseka pakubwa. Na huoni kwamba ni ngumu hata zaidi kufikiria kupitia kwa mateso ya Shetani namna ambavyo mtu atakavyopitia ambaye amekabidhiwa Shetani kabisa, ambaye yumo katika mashiko ya Shetani kabisa, ambaye amepoteza kabisa utunzaji na rehema ya Mungu, ambaye hayuko tena katika utawala wa Muumba, ambaye amenyang’anywa haki ya kumwabudu Yeye, na haki ya kuwa kiumbe katika utawala wa Mungu, ambaye uhusiano wake na Bwana wa uumbaji umekalizwa kabisa? Kuteswa kwa Ayubu na Shetani kulikwa jambo ambalo lingeonekana kwa macho ya binadamu, lakini Mungu anapomkabidhi Shetani maisha ya mtu, athari zake zitakuwa jambo ambalo mtu hawezi kufikiria. Ni sawa tu na baadhi ya watu kuweza kuzaliwa tena wakiwa ng’ombe, au punda, au baadhi ya watu wakichukuliwa kabisa, na kupagawa na roho chafu, za uovu, na kadhalika. Haya ndiyo matokeo, mwisho wa baadhi ya watu ambao Mungu anawakabidhi kwa Shetani. Kwa nje, yaonekana kwamba watu hao waliomdhihaki, waliomkashifu, kumshutumu, na kumkufuru Bwana Yesu hawakupata athari zozote. Hata hivyo, ukweli ni kwamba Mungu Anao mwelekeo wa kushughulikia kila kitu. Huenda Asitumie lugha wazi kuwaambia watu matokeo ya namna Anavyowashughulikia kila aina ya watu. Wakati mwingine Haongei kwa njia ya moja kwa moja, lakini Anafanya mambo

kwa njia ya moja kwa moja. Kwamba haongelei jambo haimaanishi kwamba hakuna matokeo—yawezekana kwamba matokeo ni mabaya zaidi. Inavyoonekana, yaelekea Mungu haongei na watu fulani ili kufichua mwelekeo Wake; kwa uhakika, Mungu hajataka kuwaza juu yao kwa muda mrefu. Hataki kuwaona tena. Kwa sababu ya mambo ambayo wamefanya, tabia yao, kwa sababu ya asili yao na kiini chao, Mungu anawataka tu watoweke machoni Mwake, Anataka kuwakabidhi moja kwa moja kwa Shetani, kumpa Shetani roho yao, nafsi yao na mwili wao, kumruhusu Shetani kufanya atakacho. Ni wazi ni hadi kiwango gani Mungu anawachukia, ni hadi kiwango gani Ameudhika nao. Kama mtu atamghadhabisha Mungu kufikia kiwango ambacho Mungu hataki kumwona tena, kwamba Atakata tamaa kabisa naye, hadi katika kiwango ambacho Mungu hataki tena kushughulika naye Yeye mwenyewe—kama itafikia kiwango hiki ambapo Atawakabidhi kwa Shetani ili aweze kufanya apendavyo, kumruhusu Shetani kumdhibiti, kumtumia, na kumtendea kwa njia yoyote—mtu huyu kwa kweli amemalizika. Haki yake ya kuwa binadamu imebatilishwa kabisa, na haki yake ya kuwa kiumbe imefikia mwisho. Je, huoni kwamba hii ndiyo adhabu mbaya zaidi?

Yote haya yaliyo hapo juu ni maelezo kamilifu ya maneno: “hatasamehewa, wala katika dunia hii, wala katika dunia itakayokuja,” na pia ni utoaji maoni mwepesi kuhusu dondoo za maandiko haya. Nafikiri kwamba mnao ufahamu wake sasa!

Sasa hebu tusome dondoo za maandiko zilizo hapa chini.

12. Maneno ya Yesu kwa Wanafunzi Wake Baada ya Kufufuka Kwake

Yohana 20:26-29 Na kufuatia siku nane tena wanafunzi wake walikuwa ndani, naye Tomaso alikuwa nao: kisha Yesu akaja, milango ikiwa imefungwa, na kusimama katikati, na kusema, Amani iwe nanyi. Kisha akasema kwa Tomaso, nyoosha kidole chako hapa, na uitazame mikono yangu, nyoosha mkono wako hapa, na u songeshe mbavuni mwangu: na usiwe bila imani, ila mwenye imani. Naye Tomaso akajibu na kumwambia, BWANA Wangu na Mungu wangu. Yesu akasema kwake, Tomaso, kwa sababu umeniona, umeamini, wamebarikiwa wale ambao hawajaona, lakini wameamini.

Yohana 21:16-17 Akasema kwake tena mara ya pili, Simioni, mwana wa Yohana, unanipenda mimi? Akasema kwake, Ndiyo, Bwana, unajua kwamba mimi nakupenda. Akasema kwake, Walishe kondoo wangu. Akasema kwake mara ya tatu, Simioni, mwana wa Yohana, Unanipenda Mimi? Petro alisikitika kwa sababu alimwambia mara ya tatu, Unanipenda Mimi? Na akamwambia, Bwana, wewe unajua vitu vyote, unajua kwamba mimi nakupenda. Yesu akamwambia, Walishe kondoo wangu.

Kile ambacho dondoo hizi zinasimulia ni baadhi ya mambo ambayo Bwana Yesu alifanya

na kusema kwa wanafunzi wake baada ya kufufuka Kwake. Kwanza, hebu tuangalie tofauti zozote kati ya Bwana Yesu kabla na baada ya kufufuka Kwake. Alikuwa bado ni yule yule Bwana Yesu wa siku za kale? Maandiko yanao mstari ufuatao unaomfafanua Bwana Yesu baada ya kufufuka kwake: “Kisha Yesu akaja, milango ikiwa imefungwa, na kusimama katikati, na kusema, Amani iwe nanyi.” Ni wazi sana kwamba Bwana Yesu wakati huo hakuwa tena mwili, lakini alikuwa katika umbo la kiroho. Hii ni kwa sababu Alikuwa amepita ile mipaka ya mwili, na wakati ambapo mlango ulifungwa Aliweza bado kuja katikati ya watu na kuwaruhusu wao kumwona Yeye. Hii ndiyo tofauti kubwa zaidi kati ya Bwana Yesu baada ya kufufuka na Bwana Yesu aliyeishi kwa mwili kabla ya kufufuka. Hata ingawa hakukuwa na tofauti yoyote kati ya kutokea kwa ule mwili wa kiroho wa wakati huo na dhihirisho la Bwana Yesu kutoka awali, Yesu katika muda huo alikuwa amekuwa Yesu aliyehisi na kujioa mgeni kwa watu, kwa sababu Alikuwa amekuwa mwili wa kiroho baada ya kufufuka kutoka kwa wafu, na Akilinganishwa na mwili Wake wa awali, mwili huu wa kiroho ulikuwa wa kushangaza na kuchanganya kwa watu zaidi. Hali hii iliunda nafasi kubwa zaidi kati ya Bwana Yesu na watu, nao watu wakahisi katika mioyo yao kwamba Bwana Yesu wa wakati huo alikuwa haeleweki kabisa. Ufahamu na hisia hizi kwa upande wa watu ghafla uliwarudisha katika enzi ya kuamini kwa Mungu ambaye hakuweza kuonekana wala kugusika. Hivyo basi, kitu cha kwanza ambacho Bwana Yesu alifanya baada ya kufufuka Kwake kilikuwa kuruhusu kila mmoja kuweza kumwona, kuthibitisha kuwa yupo, kuthibitisha hoja ya kufufuka Kwake. Kuongezea hayo, hali hiyo ilirejesha uhusiano Wake na watu hadi ule uhusiano Aliokuwa nao Alipokuwa akifanya kazi kupitia kwa mwili, na Alikuwa Kristo ambaye wangeweza kuona na kugusa. Kwa njia hii, mojawapo ya matokeo ni kwamba watu hawakuwa na shaka kwamba Bwana Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa kifo baada ya kusulubishwa msalabani, na hakukuwa na shaka katika kazi ya Bwana Yesu ya kuwakomboa wanadamu. Na matokeo mengine ni kwamba hoja ya Bwana Yesu kujitokeza kwa watu baada ya kufufuka Kwake na kuwaruhusu watu kuweza kumwona na kumgusa Yeye kwa udhabiti kuliweza kuwasalimisha wanadamu katika Enzi ya Neema. Kuanzia wakati huu, watu hawakuweza kurudi katika enzi ya awali, Enzi ya Sheria, kwa sababu ya “kutoweka” au “kuacha na kuondoka” kwa Bwana Yesu lakini wangeendelea mbele, kufuata mafundisho ya Bwana Yesu na kazi Aliyokuwa amefanya. Hivyo basi, awamu mpya katika kazi ya Enzi ya Neema iliweza kufunguliwa rasmi na watu waliokuwa katika sheria walikuja rasmi kutoka katika sheria kuanzia hapo kuenda mbele, na kuingia katika enzi mpya, katika mwanzo mpya. Hizi ndizo maana nyingi za kujitokeza kwa Bwana Yesu kwa wanadamu baada ya kufufuka Kwake.

Kwa sababu Alikuwa mwili wa kiroho, watu waliwezaje kumgusa Yeye na kumwona Yeye? Hii inahusu umuhimu wa kujitokeza kwa Bwana Yesu kwa wanadamu. Je, mlitambua

chochote katika dondoo hizi za maandiko? Kwa ujumla miili ya kiroho haiwezi kuonekana wala kuguswa, na baada ya kufufuka, kazi ambayo Bwana Yesu alikuwa amechukua tayari ilikuwa imekamilika. Hivyo basi, kinadharia Hakuwa na haja kabisa ya kurudi katikati ya watu akiwa katika taswira Yake ya asili ili kukutana na wao, lakini kujitokeza kwa mwili wa kiroho wa Bwana Yesu kwa watu kama vile Tomaso kulifanya umuhimu wake kuwa thabiti zaidi, na hali hii iliweza kupenyeza zaidi kwa kina katika mioyo ya watu. Alipomjia Tomaso, alimwacha Tomaso aliyekuwa akishuku kumgusa mkono Wake na kumwambia maneno haya: “Nyoosha mkono wako hapa, na uusongeshe mbavuni mwangu: na usiwe bila imani, ila mwenye imani.” Maneno haya, vitendo hivi vyote havikuwa vitu ambavyo Bwana Yesu alitaka kusema na kufanya tu baada ya Yeye kufufuka, lakini yalikuwa mambo Aliyotaka kuyafanya kabla ya kusulubishwa msalabani. Ni wazi kwamba Bwana Yesu ambaye alikuwa hajasulubishwa katika msalaba tayari alikuwa na ufahamu wa watu kama Tomaso. Hivyo basi, tunaweza kuona nini kutokana na haya? Alikuwa angali Bwana Yesu yule yule hata baada ya kufufuka Kwake. Kiini chake kilikuwa hakijabadilika. Kushuku kwa Tomaso hakukuwa kumeanza tu lakini kulikuwa ndani yake muda wote aliokuwa akimfuata Bwana Yesu, lakini Alikuwa Bwana Yesu aliyekuwa amefufuka kutoka kwa kifo na alikuwa amerudi kutoka katika ulimwengu wa kiroho akiwa na taswira Yake asilia, na tabia Yake binafsi, na kwa ufahamu huu wa wanadamu kutoka kwa wakati Wake akiwa mwili, kwa hivyo basi Alienda kumfuta Tomaso kwanza, ili kumfanya Tomaso kugusa mbavu Zake, kumfanya kutoona tu mwili Wake wa kiroho baada ya kufufuka, lakini pia kumruhusu auguse na kuuhisi uwepo wa mwili Wake wa kiroho, na kutupilia mbali kabisa shaka zake. Kabla ya Bwana Yesu kusulubishwa msalabani, Tomaso siku zote alishuku kwamba Yeye ni Kristo, na hakuweza kuamini. Imani yake katika Mungu ilianzishwa tu kwa msingi wa kile ambacho angeweza kuona kwa macho yake, kile ambacho angeweza kugusa kwa mikono yake. Bwana Yesu alikuwa na ufahamu mzuri wa imani ya mtu wa aina hii. Waliamini tu katika Mungu wa mbinguni, na hawakuamini kamwe, na wasingekubali Yule Aliyetumwa na Mungu, au Kristo katika mwili. Ili kufanya yeye kuweza kutambuliwa na kuaminiwa katika uwepo wa Bwana Yesu na kwamba kweli Alikuwa Mungu mwenye mwili, Alimruhusu Tomaso kuunyosha mkono wake na kugusa ubavu Wake. Je, Tomaso alikuwa akishuku kwa njia tofauti kabla na baada ya kufufuka kwa Bwana Yesu? Alikuwa daima akishuku, na mbali na mwili wa kiroho wa Bwana Yesu kujitokeza binafsi kwake na kumruhusu Tomaso kugusa alama za misumari katika mwili Wake, hakuna aliyeweza kutatua shaka zake, na hakuna mtu ambaye angemfanya kuziachilia. Hivyo basi, kuanzia muda ambao Bwana Yesu alimruhusu kuugusa ubavu Wake na kumwacha akihihi uwepo wa alama za misumari, shaka ya Tomaso ikatoweka na akajua kwa kweli kwamba Bwana Yesu alikuwa amefufuka na akatambua na kuamini kwamba Bwana Yesu ndiye aliyekuwa Kristo wa kweli, na kuamini kwamba alikuwa Mungu mwenye mwili. Ingawa wakati huu Tomaso hakushuku tena, alikuwa amepoteza milele fursa ya kukutana

na Kristo. Alikuwa amepoteza milele fursa ya kuwa pamoja na Yeye, kumfuata Yeye, na kumjua Yeye. Alikuwa amepoteza fursa ya Kristo kumfanya yeye kuwa mtimilifu. Kuonekana kwa Bwana Yesu na maneno Yake yalitoa hitimisho, na hukumu kuhusiana na imani ya wale ambao walijawa na kutoamini kwingi. Alitumia maneno na vitendo Vyake halisi kuwaambia wale waliokuwa wakishuku, kuwaambia wale ambao waliamini tu katika Mungu aliye juu mbinguni lakini amini hawakumwamini Kristo: Mungu hakuitukuza imani yao, wala Hakuupongeza ufuasi wao uliojawa na shaka. Ile siku waliamini kikamilifu Mungu naye Kristo angeweza tu kufanya hivyo siku ile ambayo Mungu alikuwa akamilishe kazi Yake kuu. Bila shaka, siku hiyo ndiyo iliyokuwa siku ambayo kushuku kwao kulipokea uamuzi. Mwelekeo wao katika Kristo uliamua majaliwa yao, na kushuku kwao katika usumbufu kulimaanisha imani yao haikuwapatia matokeo yoyote, na ugumu wao kulimaanisha matumaini yao yaliambukia patupu. Kwa sababu imani yao katika Mungu aliye mbinguni ilisababishwa na njozi, na kushuku kwao katika Kristo kulikuwa kwa kweli mwelekeo wao wa kweli kwa Mungu, hata ingawa walizigusa alama za msumari kwenye mwili wa Bwana Yesu, imani yao ilikuwa bado bure bilashi na matokeo yao yangeweza tu kufafanuliwa kama kuchota maji na kikapu cha mianzi—yote ni bure bilashi. Kile Bwana Yesu Alichomwambia Tomaso kilikuwa kikisema hivyo waziwazi kwa kila mtu: Yule Bwana Yesu aliyefufuka ndiye Bwana Yesu ambaye mwanzo alikuwa ametumia miaka thelathini na mitatu na nusu akifanya kazi miongoni mwa wanadamu. Ingawa alikuwa amesulubishwa msalabani na kupitia bonde la kivuli cha mauti, alikuwa amepitia kitendo cha kufufuka, kila dhana Yake haikuwa imepitia mabadiliko. Ingawa kwa sasa alikuwa na alama za misumari kwenye mwili Wake, na ingawa Alikuwa amefufuka na kutoka kaburini akitembea, tabia Yake, ufahamu Wake wa wanadamu na nia Zake kwa wanadamu bado zilikuwa hazijabadilika hata kidogo. Pia, Alikuwa akiwaambia watu kwamba Alikuwa ameshuka kutoka kwenye msalaba, ameshinda dhambi, amepata ushindi juu ya ugumu, na akupata ushindi dhidi ya kifo. Alama zile za misumari zilikuwa tu ithibati ya ushindi Wake dhidi ya Shetani, ithibati ya kuwa sadaka ya dhambi ili kuweza kuwakomboa kwa ufanisi wanadamu wote. Alikuwa akiwaambia watu kwamba tayari Alikuwa ameanza kushughulikia dhambi za wanadamu na Alikuwa amekamilisha kazi Yake ya ukombozi. Aliporudi ili kuwaona wanafunzi Wake, Aliwaambia kwa kuonekana Kwake: “Mimi niko hai, bado Nipo; leo kwa kweli nasimama mbele yenu ili mweze kuniona na kunigusa Mimi. Siku zote nitakuwa na wewe.” Bwana Yesu alitaka pia kutumia mfano huo wa Tomaso kama onyo kwa watu wa siku za usoni: Ingawa unaamini Bwana Yesu, huwezi kumwona wala kumgusa Yeye, na bado, unaweza kubarikiwa kutokana na imani yako ya kweli, na unaweza kumwona Bwana Yesu kupitia kwa imani yako ya kweli; mtu aina hii amebarikiwa.

Maneno haya yaliyorekodiwa katika Biblia ambayo Bwana Yesu aliongea Alipojitokeza kwa Tomaso ni msaada mkubwa kwa watu wote katika Enzi ya Neema. Kuonekana Kwake na

maneno Yake kwa Tomaso yamekuwa na athari kubwa kwa vizazi vijavyo, na yatakuwa na umuhimu wa kudumu daima dawamu. Tomaso anawakilisha mtu wa aina ya kuamini Mungu ilhali anamshuku Mungu. Wao wanayo maumbile ya kushuku, wana mioyo isiyoeleweka, wao wenyewe ni wadanganyifu, na hawaamini mambo ambayo Mungu anaweza kukamilisha. Hawaamini katika kudura ya Mungu na utawala Wake, na hawaamini katika Mungu kuwa mwili. Hata hivyo, kufufuka kwa Bwana Yesu kulikuwa ni sawa na kuzabwa kofi katika nyuso zao, na pia kuliwapa fursa ya kugundua ni shaka yao wenyewe, kutambua kushuku kwao binafsi, na kuukubali udanganyifu wao binafsi na hivyo basi kuamini katika kuwepo na kufufuka kwa Bwana Yesu. Kile kilichomfanyikia Tomaso kilikuwa onyo na tahadhari kwa vizazi vijavyo ili watu wengi zaidi waweze kujitahadharisha na ili wasiwe wa kushuku kama Tomaso, na kama wangukuwa hivyo, wangezama katika giza. Ukimfuata Mungu, lakini kama Tomaso, siku zote unataka kuugusa ubavu wa Bwana na kuhisi alama Zake za msumari ili kuthibitisha, ili kuhakikisha, ili kuchambua kama Mungu yupo, basi Mungu atakuacha. Hivyo basi, Bwana Yesu anawahitaji watu wasiwe kama Tomaso, kuamini tu kile wanachoweza kuona kwa macho yao, lakini kuwa bila kasoro, mtu mwaminifu, kutouwa na shaka yoyote dhidi ya Mungu, lakini kumwamini tu na kumfuata Yeye. Mtu wa aina hii amebarikiwa. Hili ni hitaji dogo sana la Bwana Yesu kwa watu, na onyo kwa wafuasi Wake.

Huu ndio mwelekeo wa Bwana Yesu kwa wale waliojaa shaka. Hivyo basi ni nini ambacho Bwana Yesu alimwambia, na ni nini Alichofanya kwa wale ambao wanaweza kuamini kwa uaminifu na kumfuata Yeye? Maswali hayo ndiyo tutakayoyaangalia katika kipindi kifuatacho, kuhusiana na kitu ambacho Bwana Yesu alimwambia Petro.

Katika mazungumzo haya, Bwana Yesu alimwuliza Petro mara kadhaa kuhusu jambo moja: “Simoni, mwana wa Yohana, je, unanipenda?” Hiki ndicho kiwango cha juu zaidi ambacho Bwana Yesu alihitaji kutoka kwa watu kama vile Petro baada ya kufufuka Kwake, wanaoamini Kristo kwa kweli na kulenga kumpenda Bwana. Swali hili lilikuwa aina fulani ya uchunguzi, na aina fulani ya kuhoji, lakini hata zaidi lilikuwa hitaji na tarajio la watu kama Petro. Aliitumia mbinu hii ya kuuliza maswali ili watu waweze kuwaza na kuwazua kujihusu na kuangalia katika maisha yao wenyewe: Mahitaji ya Bwana Yesu kwa watu ni yapi? Je, nampenda Bwana? Mimi ni mtu anayempenda Mungu? Nafaa vipi kumpenda Mungu? Hata ingawa Bwana Yesu aliuliza tu swali hili kwa Petro, ukweli ni kwamba katika moyo Wake, Alitaka kutumia fursa hii ya kumwuliza Petro ili kuuliza swali la aina hii kwa watu wengi zaidi wanaoutafuta kumpenda Mungu. Ni kwa sababu tu kuwa Petro alibarikiwa kuwa mwakilishi wa mtu wa aina hii, ili kupokea swali hilo kutoka kwa kinywa cha Bwana Yesu mwenyewe.

Likilinganishwa na “nyoosha mkono wako hapa, na uusongeshe mbavuni mwangu: na

usiwe bila imani, ila mwenye imani,” ambalo Bwana Yesu alimwambia Tomaso baada ya kufufuka Kwake, Yeye kumwuliza Petro swali mara tatu: “Simioni, mwana wa Yohana, unanipenda mimi?” waruhusu watu kuweza kuhisi kwa njia bora zaidi ule ukali wa mwelekeo wa Bwana Yesu na umuhimu Aliouhisi wakati huu wa kuuliza maswali hayo. Kuhusiana naye Tomaso wa kushuku pamoja na asili yake ya udanganyifu, Bwana Yesu alimruhusu yeye kufikisha mkono wake na kuzigusa zile alama Zake za msumari, jambo ambalo lilimfanya yeye kuamini kwamba Bwana Yesu ndiye aliyekuwa Mwana wa Adamu aliyefufuka na akatambua utambulisho wa Bwana Yesu kama Kristo. Na ingawa Bwana Yesu hakumkemea kwa ukali Tomaso, wala hakuonyesha kwa matamshi hukumu yoyote ilio wazi kwake, Alimjuza kwamba Alimwelewa kupitia kwa hatua za kimatendo, huku pia akionyesha mtazamo Wake na uamuzi wa aina hiyo ya mtu. Mahitaji na matarajio ya Bwana Yesu ya mtu wa aina hiyo hayawezi kuonekana kutokana na kile Alichosema. Kwa sababu watu kama Tomaso hawana katu imani ya ukweli. Mahitaji ya Bwana Yesu kwao yanapatikana tu katika, lakini mwelekeo Alioufichua kwa watu kama Petro ni tofauti kabisa. Hakuhitaji kwamba Petro aunyoshe mkono wake na kuzigusa hizo alama Zake za misumari, wala hakumwambia Petro: “usiwe bila imani, ila mwenye imani.” Badala yake, Alimwuliza Petro kwa kurudia swali lilo hilo. Hili lilikuwa swali la kuchokonoa fikira, na lenye maana ambalo halina budi kumfanya kila mfuasi wa Kristo kuhisi majuto, na woga, lakini pia kuhisi ile hali ya moyo wa wasiwasi, na huzuni ya Bwana Yesu. Na wakati wakiwa katika maumivu na mateso makali, wanaweza kuelewa zaidi wasiwasi wa Bwana Yesu Kristo na utunzaji Wake; wanatambua mafundisho Yake ya dhati na mahitaji makali kuhusu watu wasio na kasoro, waaminifu. Swali la Bwana Yesu linawaruhusu watu kuhisi kwamba matarajio ya Bwana kwa watu yaliofichuliwa kupitia kwa maneno haya mepesi si ya kuamini tu na kumfuata Yeye, lakini kutimiza yote kwa kuwa na upendo, kumpenda Bwana wako, kumpenda Mungu wako. Upendo wa aina hii ni wa utunzaji na utiifu. Ni wanadamu kuishi kwa ajili ya Mungu, kufa kwa ajili ya Mungu, kujitolea kila kitu chao kwa ajili ya Mungu, na kutumia na kutoa kila kitu chao kwa ajili ya Mungu. Upendo wa aina hii pia ni kumpa Mungu tulizo, kumruhusu Yeye kufurahia ushuhuda, na kumruhusu Yeye kupumzika. Ni fidia ya wanadamu kwa Mungu, uwajibikaji wao, na wajibu wao, na ni njia ambayo wanadamu lazima wafuate kwa maisha yao yote. Haya maswali matatu yalikuwa mahitaji na ushawishi ambao Bwana Yesu alitoa kwa Petro na watu wote ambao wangepanywa kuwa watimilifu. Ni maswali haya matatu ndiyo yaliyomwongoza na kumpa motisha Petro kukamilisha njia yake ya maisha, na yalikuwa maswali haya wakati ule wa Bwana Yesu kuondoka ambayo yalimfanya Petro kuanza njia yake ya kufanywa mtimilifu, na yaliyomwongoza, kwa sababu ya upendo wake kwa Bwana, kuutunza moyo wa Bwana, kumtii Bwana, kumpa tulizo Bwana, na kuyatoa maisha yake yote na kila kitu chake chote kwa sababu ya upendo wake.

Katika Enzi ya Neema, kazi ya Mungu ilikuwa kimsingi ya aina mbili ya watu. Wa kwanza alikuwa aina ya aliyeamini Kwake na kumfuata, ambaye angetii amri Zake, ambaye angeweza kuuvumilia msalaba na kuushikilia hadi katika njia ya Enzi ya Neema. Mtu wa aina hii angepata baraka za Mungu na kufurahia neema ya Mungu. Aina ya pili ya mtu alikuwa kama Petro, mtu ambaye angeweza kufanywa kuwa mtimilifu. Hivyo basi, baada ya Bwana Yesu kufufuka, Alifanya kwanza mambo haya mawili yenye umuhimu sana. Kwanza lilikuwa ni kwa Tomaso, na jingine lilikuwa kwa Petro. Mambo haya mawili yanawakilisha nini? Yanawakilisha nia za kweli za Mungu katika kuwaokoa binadamu? Yanawakilisha uaminifu wa Mungu kwa binadamu? Kazi Aliyoifanya na Tomaso ilikuwa ni kuwapa onyo watu wasiwe wanashuku, lakini kuamini tu. Kazi Aliyofanya na Petro ilikuwa ni kuipatia nguvu imani ya watu kama vile Petro, na kuweka wazi mahitaji ya aina hii ya watu, ili kuonyesha ni shabaha zipi wanafaa kuwa wakifuatilia.

Baada ya Bwana Yesu kufufuka, Alijitokeza kwa watu aliofikiria walifaa, Akaongea na wao, na kuwapa wao mahitaji, huku akiacha nyuma nia Zake, na matarajio Yake kwa watu. Hivi ni kusema, kama Mungu mwenye mwili, haijalishi kama ulikuwa katika wakati Wake akiwa mwili, au katika mwili wa kiroho baada ya kusulubishwa msalabani na kufufuliwa—haja Yake kwa wanadamu na mahitaji kwa wanadamu hayakubadilika. Alijali kuwahusu wanafunzi hawa kabla ya kufika msalabani; ndani ya moyo Wake, Alikuwa wazi katika hali ya kila mmoja, Alielewa upungufu wa kila mmoja, na bila shaka ufahamu Wake wa kila mtu ulikuwa namna ile ile baada ya Yeye kuaga dunia, kufufuka, na kuwa mwili wa kiroho kama hali ilivyokuwa Alipokuwa katika mwili. Alijua kwamba watu hawakuwa kwa kikamilifu na uhakika kuuhusu utambulisho Wake kama Kristo, lakini katika kipindi Chake akiwa mwili Hakuwa anatoa amri kali kuhusu watu. Lakini baada ya kufufuliwa Alijitokeza kwao, na Akawafanya wawe na hakika kabisa kwamba Bwana Yesu alikuwa amekuja kutoka kwa Mungu, kwamba Alikuwa Mungu mwenye mwili, na Alitumia hoja hiyo ya uwepo Wake na kufufuka Kwake kama maono na motisha kubwa zaidi kwa muda mrefu katika ufuatiliaji wa wanadamu. Kufufuka kwake kutoka kifo hakukuwapa nguvu tu wale wote Waliomfuata, lakini pia kuliweka katika taathira kazi Yake ya Enzi ya Neema miongoni mwa wanadamu, na hivyo basi wokovu wa injili ya Bwana Yesu katika Enzi ya Neema kwa utaratibu ukaenea katika kila pembe ya binadamu. Unaweza kusema kwamba kutokea kwa Bwana Yesu baada ya kufufuka Kwake kulikuwa na umuhimu wowote? Kama ungekuwa Tomaso au Petro wakati huo, na ukumbane na kitu hiki kimoja katika maisha yako ambacho kilikuwa na maana sana, ni athari ya aina gani ambayo kitu hicho kingekuwa nayo kwako? Je, ungeona huu kama msukumo wako katika kumfuata Mungu? Ungeona hali hii kama nguvu endeshi zako wewe kumfuata Mungu, kujaribu kumridhisha Yeye, na kufuatilia upendo wa Mungu katika maisha yako? Ungeweza kutumia jitihada za maisha yako yote ili

kueneza maono haya makubwa zaidi? Ungefanya kueneza wokovu wa Bwana Yesu kuwa kazi unayokubali kutoka kwa Mungu? Hata ingawa hamjapitia haya, zile hali mbili za Tomaso na Petro tayari zinatoshwa kwa watu wa kisasa kuwa na ufahamu wazi kuhusu mapenzi ya Mungu na kumhusu Mungu. Inaweza kusemekana kwamba baada ya Mungu kuwa mwili, baada ya Yeye binafsi kupitia maisha miongoni mwa wanadamu na kuwa na maisha ya binadamu, na baada ya Yeye kuona uharibifu wa tabia wa wanadamu na hali ya maisha ya binadamu, Mungu katika mwili alihisi kwa kina zaidi jinsi mwanadamu alikuwa asiyejiweza, mwenye masikitiko na wa kuonewa huruma. Mungu alipata huruma zaidi kwa hali ya binadamu kwa sababu ya ubinadamu Wake wakati akiishi katika mwili, kwa sababu ya silika Zake katika mwili. Hili lilimsababisha kuwa na wasiwasi mkubwa zaidi juu ya wafuasi Wake. Haya pengine ni mambo ambayo huwezi kuelewa, lakini Naweza kufafanua wasiwasi na utunzaji wa Mungu katika damu kwa kila mmojawapo wa wafuasi Wake kwa kauli hii: kujali kwingi. Hata ingawa kauli hii inatokana na lugha ya binadamu, na hata ingawa ni kauli yenye ubinadamu sana, inaonyesha kwa kweli na kufafanua hisia za Mungu kwa wafuasi Wake. Na kwa kujali kwingi kwa Mungu kwa ajili ya binadamu, kwa mkondo wa yale yote ambayo wewe umeyapitia utanza kuhisi kwa utaratibu yote haya na kuyaonja. Hata hivyo, hali hii inaweza kutimizwa tu kwa kuelewa kwa utaratibu tabia ya Mungu kwa msingi wa kufuatilia mabadiliko katika tabia yako wewe binafsi. Kuonekana kwa Bwana Yesu kulifanikisha kujali Kwake kwingi kwa minajili ya wafuasi Wake katika ubinadamu na akakupokeza kwa mwili Wake wa kiroho, au unaweza kusema uungu Wake. Kuonekana Kwake kuliwaruhusu watu kuwa na hali nyingine waliyopitia na hisia walizopitia zinazohusu kujali na utunzaji wa Mungu huku kukithibitisha kwa uthabiti kwamba Mungu Ndiye anayefungua enzi, anayeendeleza enzi, na Yeye ndiye anayetamatisha enzi. Kupitia kwa Kuonekana Kwake Aliipatia nguvu imani ya watu wote, na kupitia kwa Kuonekana Kwake alithibitishia ulimwengu hoja kwamba Yeye ni Mungu Mwenyewe. Hali hii iliwapa wafuasi Wake uthibitisho wa milele, na kupitia kwa Kuonekana Kwake pia Aliweza kufungua awamu ya kazi Yake katika enzi mpya.

13. Yesu Ala Mkate na Kuonyesha Maandiko Baada ya Kufufuka Kwake

Luka 24:30-32 Na ikatimia, alipokuwa akikaa na wao ili wale, aliuchukua mkate, na kuubariki, na akaupasua, na kuwapa. Na macho yao yakafunguka, na wakamjua, na akatoweka wasimwone. Na wakaambiana, je, Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu sisi, wakati alipokuwa akituzungumzia njiani, na wakati alipotufungulia maandiko?

14. Wanafunzi Wampa Yesu Kipande cha Samaki wa Kuokwa Ale

Luka 24:36-43 Na wakati walipokuwa wakinena hayo, Yesu mwenyewe alisimama katikati yao, na akasema kwao, Amani iwe kwenu ninyi. Lakini walikuwa na woga na hofu sana, na

wakafikiri kwamba walikuwa wameona roho. Naye akawaambia, Mbona mnasumbuka? na mbona mashaka yanaibuka mioyoni mwenu? Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kwamba ni mimi mwenyewe: Niguseni, na kuona; kwa sababu roho haina mwili na mifupa, jinsi mnavyoniona mimi nikiwa nayo. Na baada ya yeye kunena hayo, akawaonyesha mikono yake na miguu yake. Na wakati walikuwa bado hawajaamini kwa furaha, na wakishangaa, akawaambia, Mnacho chakula chochote huku? Na wakampa kipande cha samaki wa kuokwa kwa asali. Na akakichukua, na kukila mbele yao.

Halafu tutaangalia dondoo zilizo hapo juu. Dondoo ya kwanza inamulika upya ulaji wa mkate na Bwana Yesu na unaeleza maandiko baada ya kufufuka Kwake na dondoo ya pili inaonyesha upya Bwana Yesu akila kipande cha samaki aliyekaushwa. Ni aina gani ya msaada ambao dondoo hii mara mbili inatupa kwa kuijua tabia ya Mungu? Unaweza kuwaza ni picha ya aina gani unayopata kutoka katika ufafanuzi huu wa Bwana Yesu akila mkate na kisha kipande cha samaki aliyekaushwa? Unaweza kufikiria, kama Bwana Yesu alikuwa Amesimama mbele yako wewe ukila mkate, unaweza kuhisi vipi? Au kama Angekuwa Akila pamoja nawe kwenye meza moja, huku Akila samaki kwa mkate na watu, ni hisia aina gani ambayo ungekuwa nayo wakati huo? Kama unahisi ungekuwa karibu sana na Bwana, kwamba yuko karibu sana na wewe, basi hisia yako i sahihi. Hivi ndivyo hasa tokeo ambalo Bwana Yesu alitaka kulileta kutokana na kula Kwa mkate na samaki mbele ya umati wa watu uliokusanyika baada ya kusulubishwa Kwake. Kama Bwana Yesu angekuwa ameongea tu na watu baada ya kufufuka Kwake, kama wasingeweza kuhisi mwili na mifupa Yake, lakini walihisi Alikuwa roho isiyoweza kufikika, wangehisi vipi? Hawangesikitishwa? Wakati watu wangesikitishwa, hawangehisi kwamba wameachwa? Hawangehisi ule umbali wa Bwana Yesu Kristo? Ni athari hasi ya aina gani ambayo umbali huu ungeweza kujenga katika uhusiano wa watu na Mungu? Watu wangehisi woga bila shaka, kwamba wasingethubutu kusonga karibu na Yeye, na wangukuwa na mwelekeo wa kumweka kwa mbali kiasi. Kuanzia hapo mpaka leo, wangekatiza uhusiano wao wa karibu na Bwana Yesu Kristo, na kurudi katika uhusiano kati ya wanadamu na Mungu aliye juu mbinguni, kama ilivyokuwa kabla ya Enzi ya Neema. Mwili wa kiroho ambao watu wasingeweza kuugusa au kuuhisi ungesababisha ukomeshaji wa ukaribu wao na Mungu, na ungefanya ule uhusiano wa karibu—ulioanzishwa wakati Bwana Yesu Kristo akiwa mwili bila ya umbali wowote kati Yake yeye na binadamu—ukose kuwepo. Hisia za watu kwa mwili wa kiroho ni za woga tu, kuepuka, na mtazamo usioeleweka. Hawathubutu kukaribia zaidi au kuwa na mazungumzo na Yeye, sikuumbii hata kufuata, kuwa na imani, au kuwa na matumaini Kwake. Mungu hakupenda kuiona hisia ya aina hii ambayo wanadamu walikuwa nayo kwake Yeye. Hakutaka kuwaona watu wakimwepuka Yeye au wakijiondoa Kwake yeye; Aliwataka tu watu kumwelewa Yeye, kumkaribia na kuwa familia Yake. Kama familia yako binafsi, watoto

wako wangekuona lakini wasingekutambua wewe, na hawakuthubutu kukukaribia lakini siku zote walikuepuka wewe, kama usingeweza kupata ufahamu wao kwa kila kitu ulichokuwa umewafanyia, ungehisi vipi? Halingekuwa jambo la uchungu? Je, hungevunjika moyo? Hivyo hasa ndivyo Mungu anavyohisi wakati watu wanamwepuka. Hivyo basi, baada ya kufufuka Kwake, Bwana Yesu bado alijitokeza kwa watu katika umbo Lake la mwili na damu, na kula na kunywa pamoja nao. Mungu huwaona watu kama familia na pia anataka wanadamu kumwona Yeye kwa njia hiyo; ni kwa njia hii tu ndivyo Mungu anavyoweza kuwapata watu kwa kweli, na ndio watu wanavyoweza kumpenda na kumwabudu Mungu kwa kweli. Sasa mnaweza kuelewa nia Yangu katika kudondoa dondoo hizi mbili kutoka katika maandiko pale ambapo Bwana Yesu anaula mkate na kuonyesha maandiko baada ya kufufuka Kwake, na wanafunzi wanampa kipande cha samaki aliyechomwa ale?

Inaweza kusemekana kwamba misururu ya mambo ambayo Bwana Yesu alisema na kufanya baada ya kufufuka Kwake yalikuwa ya fikira njema, na kufanywa kwa nia njema. Walijaa huruma na huba ambayo Mungu alishikilia kwa binadamu, na akiwa amejaa pia na mapenzi na utunzaji wa makini Aliokuwa nao kwa minajili ya uhusiano wa karibu aliokuwa Ameanzisha na wanadamu wakati Akiwa katika mwili. Hata zaidi walijaa kumbukumbu za kitambo na tamaa Alilokuwa nayo kutokana na maisha Yake ya kula na kuishi miongoni mwa wafuasi Wake wakati akiwa katika mwili. Hivyo basi, Mungu hakuwataka watu kuhisi umbali kati ya Mungu na binadamu, wala Hakutaka wanadamu kuwa mbali na Mungu. Hata zaidi, Hakutaka wanadamu wahisi kwamba Bwana Yesu baada ya kufufuka Kwake hakuwa tena Bwana ambaye alikuwa wa karibu na watu, kwamba Hakuwa pamoja tena na wanadamu kwa sababu Alirudi katika ulimwengu wa kiroho, alirudi kwa Baba ambaye watu wengi wasingeweza kumwona wala kumsikia. Hakutaka watu kuhisi kwamba kulikuwa na tofauti yoyote katika cheo kati Yake na wanadamu. Mungu anapowaona watu wanaotaka kumfuata lakini wanamweka katika umbali fulani, moyo Wake unapata maumivu kwa sababu hiyo inamaanisha kwamba mioyo yao iko mbali sana na Yeye, inamaanisha kwamba itakuwa vigumu sana Kwake yeye kuweza kuipata mioyo yao. Hivyo basi kama angekuwa amejitokeza kwa watu kupitia kwa mwili wa kiroho ambao wasingeweza kuuona ama kuugusa, hali hii kwa mara nyingine tena ingeweza kumweka binadamu mbali na Mungu, na ingewasababisha wanadamu kumwona Kristo kimakosa baada ya kufufuka Kwake kuonekana kuwa Amegeuka kuwa na majivuno, wa aina tofauti na wanadamu, na mtu ambaye asingeweza tena kushiriki meza na kula pamoja na binadamu kwa sababu wanadamu ni wenye dhambi, wananuka, na hawawezi kumkaribia Mungu hata kidogo. Ili kuondoa kutoelewana huku kwa wanadamu, Bwana Yesu alifanya mambo kadha wa kadha ambayo mara kwa mara Alifanya katika mwili, kama ilivyorekodiwa katika Biblia, “aliuchukua mkate, na kuubariki, na akaupasua, na kuwapa.” Pia Aliwachambulia maandiko,

kama Alivyokuwa amezoea kufanya. Yote haya ambayo Bwana Yesu alifanya yalimfanya kila mmoja aliyemwona Yeye kuhisi kwamba Bwana hakuwa amebadililika, kwamba alikuwa bado Bwana Yesu. Hata ingawa Alikuwa amesulubishwa msalabani na kupitia kifo, Alikuwa amefufuliwa, na hakuwa amemwacha binadamu. Alikuwa amerudi kuwa miongoni mwa wanadamu, na kila kitu Chake hakikuwa kimebadilika. Mwana wa Adamu akiwa amesimama mbele ya watu alikuwa bado Bwana Yesu. Mwenendo Wake na mazungumzo Yake na watu yalikuwa ya kawaida sana. Alikuwa angali bado na huruma na upendo, neema, na uvumilivu—Alikuwa bado Bwana Yesu aliyewapenda wengine kama Alivyojipenda Mwenyewe, ambaye angeweza kuwasamehe wanadamu mara sabini mara saba. Kama kawaida, Alikula na watu, kuzungumza maandiko na wao, na hata muhimu zaidi, sawa tu na kama alivyofanya awali, Alifanywa kuwa mwili na damu na aliweza kuguswa na kuonekana. Mwana wa Adamu katika njia hii aliwaruhusu watu kuhisi upendo huo, kuhisi kuwa watulivu, na kuhisi furaha ya kupata tena kitu ambacho kilikuwa kimepotea, na wao pia walihisi watulivu kwa njia tosha ya kuanza kumtegemea na kumtumainia Mwana huyu wa Adamu kwa ujasiri na kwa imani ambaye angeweza kuwasamehe wanadamu dhambi zao. Walianza pia kuomba katika jina la Bwana Yesu bila ya kusita, kuomba ili kupokea neema Yake, baraka Zake, na kupokea amani na furaha kutoka Kwake, kupata utunzaji na ulinzi kutoka Kwake na kuanza kutenda uponyaji na kupunga mapepo kwa jina la Bwana Yesu.

Katika muda huu ambao Bwana Yesu alifanya kazi katika mwili, wengi wa wafuasi Wake wasingeweza kuthibitisha kikamilifu utambulisho Wake na mambo Aliyoyasema. Wakati aliposulubishwa msalabani, mwelekeo wa wafuasi Wake ulikuwa ule wa matarajio; aliposulubiwa msalabani na kupitishiwa yale yote aliyopitishiwa hadi alipowekwa katika kaburi, mwelekeo wa watu Kwake yeye ulikuwa wa kutoridhika. Wakati huu, watu walikuwa tayari wameanza kusonga katika mioyo yao kutoka katika kushuku hadi kukataa mambo ambayo Bwana Yesu alikuwa amesema wakati Akiwa mwili. Na Alipotembea nje ya kaburi na kujitokeza kwa watu mmoja baada ya mwingine, wengi wa watu ambao walikuwa wamemwona Yeye kwa macho yao au kusikia habari za kufufuka Kwake, walibadilika kwa utaratibu kutoka katika hali ya kumkataa hadi ile ya nadharia ya kushuku. Kufikia muda ule ambao Bwana Yesu alimfanya Tomaso kuuweka mkono wake katika upande Wake, kufikia wakati ambao Bwana Yesu aliuvunja mkate na kuula mbele ya umati wa watu baada ya kufufuka Kwake na baada yake kula kipande cha samaki aliyechemshwa mbele yao, hapo tu ndipo walipokubali kwa kweli Bwana Yesu ni Kristo katika mwili. Mnaweza kusema kwamba ni kana kwamba mwili huu wa kiroho ulio na nyama na damu uliosimama mbele ya hao watu ulikuwa ukizindua kila mmoja wao kutoka katika ndoto. Mwana wa Adamu akiwa amesimama mbele yao Ndiye aliyekuwepo tangu miaka hiyo ya nyuma. Alikuwa na umbo, na mwili, na mifupa, na Alikuwa tayari ameishi

na kula na wanadamu kwa muda mrefu.... Wakati huu, watu walihisi kwamba uwepo Wake ulikuwa halisi, wa ajabu sana; wote walichangamka na kufurahi mno, na wakati uo huo walijawa na hisia. Na kuonekana Kwake tena kuliwaruhusu watu waweze kuona kwa kweli unyenyekevu Wake, kuhisi ukaribu Wake na tamanio Lake, uhusiano Wake wa karibu na wanadamu. Kupatana huku kwa kufupi kuliwafanya watu waliomwona Bwana Yesu kuhisi kana kwamba muda mrefu umepita. Mioyo yao iliyopotea, kuchanganyikiwa, yenye woga, yenye wasiwasi, inayotarajia na isiyosikia hisia zozote vyote vilipata utulivu. Hawakuwa na shaka tena au kutoridhika tena kwa sababu walihisi kwamba sasa kulikuwa na tumaini na kitu cha kutegemea. Mwana wa Adamu akiwa amesimama mbele yao Angekuwa nao milele, Angekuwa mnara wao dhabiti, kimbilio lao la kila wakati.

Ingawa Bwana Yesu alifufuliwa, moyo Wake na kazi Yake vyote havikuwa vimeondoka kwa wanadamu. Aliwaambia watu Alipoonekana ya kwamba haijalishi ni umbo gani Alilokuwemo ndani, Angeandamana na watu, kutembea na wao, na kuwa na wao siku zote na katika sehemu zote. Na nyakati zote na mahali popote, Angewatosheleza wanadamu na kuwachunga, kuwaruhusu kumgusa na kumwona Yeye, na kuhakikisha kwamba hawatawahi kuhisi tena kama wasio na msaada. Bwana Yesu alitaka pia watu wajue yafuatayo: Maisha yao ulimwenguni hawapo pekee. Mwanadamu ana utunzaji wa Mungu, Mungu yuko pamoja nao; watu siku zote wanaweza kumwegemea Mungu; Yeye ndiye familia ya kila mmoja wa wafuasi Wake. Akiwa na Mungu wa kumwegemea, mwanadamu hatawahi tena kuwa mpweke au bila usaidizi, na wale wanaomkubali kama sadaka yao ya dhambi hawataishia katika dhambi tena. Katika macho ya binadamu, sehemu hizi za kazi Zake ambazo Bwana Yesu alitekeleza baada ya kufufuka Kwake zilikuwa chache mno lakini Ninavyoona Mimi, kila kitu kilikuwa na maana yenye thamani sana na zote zilikuwa zenye umuhimu na uzito.

Ingawa muda wa Bwana Yesu kufanya kazi katika mwili ulijaa ugumu na mateso, kupitia katika kuonekana Kwake katika mwili Wake wa kiroho wa mwili na damu, Alikamilisha vyema na kwa njia timilifu kazi Yake ya wakati huo akiwa kwa mwili ili kuwakomboa wanadamu. Aliianza huduma Yake kwa kugeuka mwili na Alihitimisha huduma Yake kwa kujitokeza kwa wanadamu Akiwa katika umbo Lake la mwili. Alikuwa mjumbe wa Enzi ya Neema, Alianzisha Enzi ya Neema kupitia kwa utambulisho Wake kama Kristo. Kupitia utambulisho Wake kama Kristo, Alitekeleza kazi katika Enzi ya Neema na Akaipatia nguvu na kuwaongoza wafuasi katika Enzi ya Neema. Inaweza kusemwa kuhusu kazi ya Mungu kwamba kwa kweli Yeye humaliza kazi Anayoianza. Kunazo hatua na mpango, na umejaa hekima ya Mungu, kudura Yake, na matendo Yake ya ajabu. Umejaa pia upendo na rehema za Mungu. Bila shaka, uzi mkuu unaotiririka katika kazi yote ya Mungu ni utunzaji Wake kwa binadamu; umejawa na hisia Zake za kujali ambazo Hawezi kuweka pembeni. Katika aya hizi za Biblia, katika kila kitu

ambacho Bwana Yesu alifanya baada ya kufufuka Kwake, kile kilichofichuliwa kilikuwa ni matumaini yasiyobadilika ya Mungu na kujali Kwake kwa wanadamu, pamoja na utunzaji wa Mungu wenye umakinifu na kuwathamini wanadamu. Mpaka sasa hakuna chochote kati ya hivi vyote ambacho kimebadilika—unaweza kukiona? Unapoviona hivi, moyo wako haugeuki bila kusukumwa na kuwa karibu na Mungu? Kama uliishi katika enzi hiyo na Bwana Yesu Akakuonekana baada ya kufufuka Kwake, kwa njia ya kushikika ili wewe uweze kuona, na kama Aliketi mbele yako, Akala mkate na samaki na kukuchambulia wewe maandiko, Akaongea na wewe, basi ungehisi vipi? Ungehisi furaha? Je, ungehisi kuwa mwenye hatia? Kutoelewana kwa awali na kuepuka Mungu kwa awali, migogoro na shaka dhidi ya Mungu—hivi vyote havingetoweka tu? Je, unadhani kwamba uhusiano kati ya binadamu na Mungu ungekuwa bora zaidi?

Kupitia kwa ufasiri wa sura hizi finyu za Biblia, uligundua makosa yoyote katika tabia ya Mungu? Uligundua uchafuzi wowote katika upendo wa Mungu? Uliuona udanganyifu au uovu wowote katika kudura ya Mungu au hekima? Bila shaka la! Sasa unaweza kusema kwa uhakika kwamba Mungu ni mtakatifu? Unaweza kusema kwa uhakika kwamba hisia za Mungu zinafichua kiini Chake na tabia kwa ujumla? Natumai kwamba baada ya kuyasoma maneno haya, kile ambacho umeelewa kutoka katika maneno haya kitakusaidia na kukufaidi katika ufuatiliaji wako wa mabadiliko katika tabia na hali ya kumcha Mungu. Natumai pia kwamba maneno haya yataweza kukuzalia matunda ambayo yatakua kila siku, hivyo basi katika mchakato wa ufuatiliaji huu kukuleta karibu na Mungu zaidi na zaidi, wa kukuleta karibu na karibu zaidi na kiwango ambacho Mungu anahitaji, ili usichoke tena na ufuatiliaji wa ukweli na usihisi tena kwamba ufuataji wa ukweli na ule wa mabadiliko katika tabia ni usumbufu au jambo duni. Ni, kwa kweli, udhihirisho wa tabia ya kweli ya Mungu na kiini kitakatifu cha Mungu ambayo yanakupa motisha kutamani mwangaza, kutamani haki, na kuazimia kufuatilia ukweli, kufuatilia ridhaa ya mapenzi ya Mungu, na kuwa binadamu anayepatwa na Mungu, na kuwa mtu halisi.

Leo tumezungumzia baadhi ya mambo ambayo Mungu alifanya katika Enzi ya Neema wakati ambapo Alikuwa mwili kwa mara ya kwanza. Kutoka kwa mambo haya, tumeona tabia ambayo Alionyesha na kuifichua katika mwili, pamoja na kila kipengele cha kile Alichacho na kile Alichacho. Vipengele hivi vyote vya kile Alichacho nacho na kile Alichacho vinaonekana kuhisishwa mno, lakini uhalisi ni kwamba kiini cha kila Alichofichua na kuonyesha hakiwezi kutenganishwa na tabia Yake mwenyewe. Kila mbinu na kila dhana ya Mungu mwenye mwili inaonyesha tabia Yake katika ubinadamu na imeunganishwa bila kutenganishwa katika kiini Chake Mwenyewe. Hivyo, ni muhimu sana kwamba Mungu alikuja kwa wanadamu kwa njia ya kuwa mwili na kazi aliyofanya katika mwili ni muhimu sana pia. Na, tabia Aliyoifichua na

mapenzi Alionyesha ni muhimu hata sana kwa kila mtu anayeishi katika mwili, kwa kila mtu anayeishi katika upotovu. Je, hili ni jambo ambalo unaweza kuelewa? Baada ya kuelewa tabia ya Mungu na kile Alichu nacho na kile Alichu, umefanya hitimisho lolote kuhusiana na namna unavyofaa kumtunza Mungu? Katika kulijibu swali hili, kwa hitimisho Ningependa kukupa onyo tatu: Kwanza, usimjaribu Mungu. Haijalishi ni kiasi kipi unachoelewa kuhusu Mungu, haijalishi ni kiwango kipi unachojua kuhusu tabia Yake, kwa vyovyote vile usimjaribu Yeye. Pili, usishindane na Mungu kuhusiana na hadhi. Haijalishi ni aina gani ya hadhi ambayo Mungu anakupa au ni kazi ya aina gani Anayokuaminia kuifanya, haijalishi ni wajibu wa aina gani ambao Atakuinua ili utende, na haijalishi ni kiasi kipi ambacho umegharimika au kujitolea kwa ajili Mungu, kwa vyovyote vile usishindane na Mungu kwa hadhi. Tatu, usishindane na Mungu. Haijalishi kama unaelewa au kama unaweza kutii kile ambacho Mungu anafanya na wewe, kile Anachopanga na wewe, na mambo Anayokuletea wewe, kwa vyovyote vile usishindane na Mungu. Kama unaweza kutekeleza onyo hizi tatu, basi utakuwa salama kwa kiasi fulani, na hutamghadhabisha Mungu kwa urahisi. Hayo ndiyo yote ya kushiriki kwa siku ya leo.

Novemba 23, 2013

Tanbihi:

a. “Laana ya kukaza na mshipi” ni laana inayotumiwa na mtawa Tang Sanzang katika riwaya ya Kichina iitwayo Safari kwenda Magharibi. Anatomia laana hii kumdhibiti Sun Wukong kwa kukaza mshipi wa chuma kwenye kichwa chake, ukimpa maumivu makali ya kichwa, na hivyo kumdhibiti. Imekuwa istiaira ya kuelezea kitu kinachomfunga mtu.

b. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee I

Mamlaka ya Mungu (I)

Vikao vyangu mbalimbali vya ushirika vilivyopita vilikuwa vinahusu kazi ya Mungu, tabia ya Mungu, na Mungu Mwenyewe. Baada ya kuvisikiliza vikao hivi vya ushirika, je, unahisi kuwa umefaidi na kupata ufahamu na maarifa kuhusu tabia ya Mungu? Ufahamu wako na maarifa ni mkubwa kiwango gani? Je, unaweza kuweka nambari katika kiwango hicho? Je, vikao hivi vya ushirika vilikupa ufahamu wa kina kuhusu Mungu? Inaweza kusemwa ufahamu huu ni maarifa ya kweli ya Mungu? Inaweza kusemwa kwamba maarifa na ufahamu huu wa Mungu ni maarifa ya hali halisi nzima ya Mungu, na kila kitu Anacho na alichu? La, bila shaka haiwezi kusemwa hivyo! Hii ni kwa sababu vikao hivi vya ushirika vilitupa tu ufahamu wa sehemu ya tabia ya Mungu, na kile Anacho na alichu—na wala si kila kitu, au uzima Wake wote. Vikao hivi vya ushirika vilikuwezesha wewe kuelewa sehemu ya kazi iliyowahi kufanywa na Mungu, na kupitia kwa hayo uliweza kuielewa tabia ya Mungu, na kile Anacho, na alichu, pamoja na

mtazamo na kufikiria kuliko kila kitu ambacho Amefanya. Hata hivyo huu ni ufahamu tu wa moja kwa moja, wa matamshi, na katika moyo wako, unabakia kutojua ni kiwango kipi haswa ambacho ni kweli. Ni nini hasa huamua kama kuna uhalisia wowote katika ufahamu wako wa mambo kama haya? Yanaamuliwa na kiwango kipi cha maneno na tabia ya Mungu ambayo kwa kweli umepitia kwenye yale yote ya kweli ambayo wewe umepitia, na kiwango kipi ambacho umeweza kuona na kujua kwenye hali hizi halisi ambazo ulipitia. “Vikao mbalimbali vya mwisho vya ushirika vilituruhusu kuelewa mambo yanayofanywa na Mungu, fikira za Mungu, na, zaidi ya yote, mtazamo wa Mungu kwa mwanadamu na msingi wa hatua Zake, pamoja na kanuni za vitendo Vyake. Na kwa hivyo tumekuja kuelewa tabia ya Mungu, na kujua Mungu kwa uzima Wake.” Je, kunaye aliyesema maneno haya? Ni sahihi kusema hivi? Kwa kweli ni wazi kwamba si sahihi. Na kwa nini Nasema kwamba si sahihi? Tabia ya Mungu, na kile Anacho na alichio, vyote vinaonyeshwa katika mambo ambayo Yeye amefanya na maneno ambayo Yeye ametamka. Binadamu anaweza kuelewa kile Anacho na alichio kupitia kwa kazi ambayo Yeye amefanya na maneno ambayo Yeye ameongea, lakini hii ni kusema tu kwamba ile kazi na maneno humwezesha binadamu kuelewa sehemu ya tabia ya Mungu, na sehemu ya kile Anacho na alichio. Kama binadamu atataka kufaidi ufahamu mwingi zaidi na ulio wazi kuhusu Mungu, basi binadamu lazima apitie maneno na kazi nyingi zaidi za Mungu. Ingawa binadamu hufaidi tu ufahamu kiasi wa Mungu wakati anapokuwa akipitia sehemu ya maneno au kazi ya Mungu, je, ufahamu huu wa kiasi unawakilisha tabia ya kweli ya Mungu? Je, unawakilisha hali halisi ya Mungu? Bila shaka unawakilisha tabia ya kweli ya Mungu, na kiini cha Mungu; hapo hapana shaka. Haijalishi ni lini au wapi, au ni kwa njia gani ambayo Mungu hufanya kazi Yake, au ni umbo gani ambalo humwonekana binadamu, au ni kwa njia gani Anaonyesha mapenzi Yake, kila kitu Anachofichua na kuonyesha huwakilisha Mungu Mwenyewe, kiini Mungu, na kile Anacho na alichio. Mungu hutekeleza kazi Yake na kile Anacho na alichio, na katika utambulisho Wake wa kweli; Huu ni ukweli mtupu. Ilhali, leo, watu wanao ufahamu kiasi tu wa Mungu kupitia maneno Yake, na kupitia kile wanachosikia wanaposikiliza mahubiri, na kwa hivyo hadi kufikia kiwango fulani, ufahamu huu unaweza kusemwa tu kuwa maarifa ya kinadharia. Kwa mtazamo wa hali zenu halisi, mnaweza kuthibitisha tu ufahamu au maarifa ya Mungu ambayo mmesikia, kuona, au kujua na kuelewa katika moyo wako leo kama kila mmoja wenu atashuhudia haya kupitia kwa yale yote halisi aliyoyapitia, na anakuja kuyajua kidogokidogo. Kama Singeweza kushiriki maneno haya na wewe, je, ungeweza kutimiza maarifa ya kweli ya Mungu ukiwa pekee kupitia kwa yale yote uliyoyapitia? Kufanya hivyo, Naogopa, kunaweza kuwa vigumu sana. Hiyo ni kwa sababu lazima watu wawe kwanza na maneno ya Mungu ili kujua namna ya kuyapitia. Hata hivyo wingi wa maneno ya Mungu ambayo watu hushiriki, hicho ndicho kiwango wanachoweza kupitia. Maneno ya Mungu huongoza njia iliyo mbele, na humpa binadamu mwongozo katika yale yote anayoyapitia. Kwa ufupi, kwa wale walio na

baadhi ya mambo ya kweli waliyoyapitia, vikao hivi mbalimbali vya mwisho vitawasaidia kutimiza ufahamu wa kina wa kweli, na hali yenye uhalisia zaidi kuhusu maarifa ya Mungu. Lakini kwa wale wasiokuwa na hali yoyote ya kweli ya waliyoipitia, au ambao wameanza tu hali yao wanayopitia, au wameanza tu kugusia uhalisia wa mambo, huu ni mtihani mkubwa.

Yale maudhui makuu ya vikao mbalimbali vya mwisho vya ushirika yalihusu “tabia ya Mungu, kazi ya Mungu, na Mungu Mwenyewe.” Ni nini ulichoona kwenye sehemu zile muhimu na kuu kati ya kila kitu Nilichoongea? Kupitia kwenye vikao hivi vya ushirika, unaweza kutambua kwamba Yule aliyefanya kazi, na Akaweza kufichua tabia hizi, ndiye Mungu Mwenyewe wa kipekee, aliye na ukuu juu ya mambo yote? Kama jibu lako ni ndiyo, basi ni nini kinachokuongoza katika hitimisho kama hilo? Katika kufikia hitimisho hili, ulizingatia vipengele vingapi? Je, kunaye yeyote anayeweza kuniambia Mimi? Ninajua kwamba vikao vya mwisho vya ushirika vilikuathiri kwa undani, na vilikupa mwanzo mpya katika moyo wako kwa minajili ya maarifa yako kwa Mungu, jambo ambalo ni kuu. Lakini Ingawa umeweza kuchukua hatua kubwa katika ufahamu wako wa Mungu ukilinganishwa na awali, ufafanuzi wako wa utambulisho wa Mungu bado unahitaji hatua zaidi ya majina ya Yehova Mungu wa Enzi ya Sheria, Bwana Yesu wa Enzi ya Neema, na Mwenyezi Mungu wa Enzi ya Ufalme. Hivi ni kusema kwamba, Ingawa vikao hivi vya ushirika kuhusu “tabia ya Mungu, kazi ya Mungu, na Mungu Mwenyewe” viliweza kukupa ufahamu fulani wa maneno yaliyowahi kuzungumzwa na Mungu, na kazi iliyowahi kufanywa na Mungu, na uwepo na vinavyomilikiwa vilivyowahi kufichuliwa na Mungu, huwezi kutoa ufafanuzi wa ukweli na mpangilio sahihi wa neno “Mungu.” Na wala huna mpangilio wa kweli na sahihi na maarifa ya hali na utambulisho wa Mungu Mwenyewe, hii ni kusema, katika hadhi ya Mungu miongoni mwa mambo yote na kote kote kwenye ulimwengu mzima. Hii ni kwa sababu, kwenye vikao vya ushirika vya awali kuhusu Mungu Mwenyewe na tabia ya Mungu, maudhui yote yalitokana na maonyesho na ufunuo mbalimbali wa awali kuhusu Mungu uliorekodiwa kwenye Biblia. Ilhali ni vigumu kwa binadamu kugundua uwepo na miliki ambazo zinamilikiwa na kuonyeshwa na Mungu wakati wa, au nje ya, usimamizi na wokovu Wake kwa mwanadamu. Kwa hivyo, hata kama utaelewa nafsi na miliki za Mungu ambazo zilifichuliwa kwenye kazi Aliyowahi kufanya, ufafanuzi wako wa utambulisho na hadhi ya Mungu ungali mbali sana na ule wa Mungu wa kipekee, Yule anayeshikilia ukuu juu ya viumbe vyote, na ni tofauti na ule wa Muumba. Vikao mbalimbali vya mwisho vya ushirika vilifanya kila mmoja kuhisi kwa njia moja: Binadamu angejuaje fikira za Mungu? Kama kweli mtu angejua, basi mtu huyo bila shaka angekuwa Mungu, kwa maana Mungu Mwenyewe ndiye anayejua fikira Zake, na Mungu Mwenyewe tu ndiye anayejua msingi na mtazamo wa kila kitu Anachofanya. Yaonekana ya kueleweka na ya mantiki kwako wewe kutambua utambulisho wa Mungu kwa njia kama hiyo, lakini ni nani anayeweza kujua kutoka

kwenye tabia na kazi ya Mungu kwamba kwa kweli hii ni kazi ya Mungu Mwenyewe, na wala si kazi ya binadamu, kazi ambayo haiwezi kufanywa kwa niaba ya Mungu na binadamu? Nani anayeweza kuona kwamba kazi hii inapatikana katika uongozi wa ukuu wa Yule aliye na hali halisi na nguvu za Mungu? Hii ni kusema kwamba, kupitia sifa au hali halisi gani ndipo unapotambua kwamba Yeye ni Mungu Mwenyewe, aliye na utambulisho wa Mungu, na Ndiye aliye na ukuu juu ya viumbe vyote? Umewahi kufikiria hivi? Kama hujawahi, basi hii inathibitisha hoja moja: Vikao mbalimbali vya mwisho vya ushirika vimeweza kukupa tu ufahamu fulani wa kipande cha historia ambapo Mungu alifanya kazi Yake, na mtazamo, maonyesho, na ufunuo wa Mungu kwenye kipindi cha kufanyika kwa kazi hiyo. Ingawa ufahamu kama huo unafanya kila mmoja wenu kutambua bila ya shaka yoyote kwamba Yule aliyetekeleza awamu hizi mbili za kazi ni Mungu Mwenyewe ambaye tunamsadiki na kumfuata, na Ndiye lazima siku zote tumfuate, tungali hatuna uwezo wa kutambua kwamba Yeye ni Mungu aliyekuwepo tangu kuumbwa kwa ulimwengu, na Atakayeendelea kuwepo milele hadi milele, na wala hatuwezi kutambua kwamba Yeye Ndiye anayetuongoza na Anayeshikilia utawala juu ya wanadamu wote. Kwa kweli hujawahi kufikiria kuhusu tatizo hili. Awe ni Yehova au Bwana Yesu, ni kupitia kwa dhana zipi za hali halisi na maonyesho husika ndipo unaweza kutambua kwamba Yeye si Mungu tu ambaye lazima umfuate, lakini pia Ndiye anayeamuru mwanadamu na Anayeshikilia ukuu juu ya hatima ya mwanadamu, ambaye, vilevile, ndiye Mungu Mwenyewe wa kipekee anayeshikilia ukuu dhidi ya mbingu na ardhi na viumbe vyote? Ni kupitia kwenye njia gani ndipo unapotambua kwamba Yule unayemsadiki na kumfuata ni Mungu Mwenyewe anayeshikilia ukuu juu ya viumbe vyote? Ni kupitia kwenye njia gani ndipo unapounganisha Mungu unayemsadiki na Mungu anayeshikilia ukuu juu ya hatima ya mwanadamu? Ni nini kinachokuruhusu kutambua kwamba Mungu unayemsadiki ndiye yule Mungu Mwenyewe wa kipekee, aliye mbinguni na ulimwenguni, na miongoni mwa viumbe vyote? Hili ndilo tatizo ambalo Nitatatua kwenye sehemu ijayo.

Matatizo ambayo hujawahi kufikiria kuhusu au huwezi kufikiria kuhusu ndiyo yayo hayo ambayo yanaweza kuwa muhimu zaidi kwa kumjua Mungu, na ambayo kwayo unaweza kutafuta ukweli usioweza kufikirika kwa mwanadamu. Wakati matatizo haya yanapokukumba, na lazima wewe ndiwe unayefaa kuyakabili, na unahitajika kufanya uamuzi, kama hutaweza kuyatatua kikamilifu kwa sababu ya ujinga au kutojua kwako, au kwa sababu yale yote uliyopitia wewe ni ya juujuu sana na unakosa maarifa ya kweli ya Mungu, basi yatakuwa kizuizi kikubwa zaidi na changamoto kubwa zaidi kwenye njia yako ya kumsadiki Mungu. Na kwa hivyo Nahisi kwamba tunahitajika kabisa kushiriki pamoja nanyi mada hii. Je, unajua tatizo lako ni nini sasa? Je, unatambua matatizo Ninayoyazungumzia? Je, matatizo haya ndiyo utakayokabiliana nayo? Je, haya ndiyo matatizo usiyoyaelewa? Je, haya ndiyo matatizo ambayo hayajawahi kukutokea? Je,

matatizo haya ni muhimu kwako? Je, ni matatizo kweli? Suala hili ni chanzo cha mkanganyo mkuu kwenu, ambalo linaonyesha kwamba hamna ufahamu wa kweli wa Mungu mnayemsadiki, na kwamba hamchukulii Yeye kwa umakinifu. Baadhi ya watu husema, “Ninajua Yeye ni Mungu, na kwa hivyo ninamfuata Yeye kwa sababu maneno Yake ni maonyesho ya Mungu. Hayo yanatosha. Thibitisho lipi zaidi linahitajika? Kwa kweli hatuhitaji kuibua shaka kuhusu Mungu? Kwa kweli hatupaswi kumjaribu Mungu? Kwa kweli hatuhitaji kuulizia hali halisi ya Mungu na utambulisho wa Mungu Mwenyewe?” Bila kujali kama unafikiria kwa njia hii, huwa Siyaulizi maswali fulani ili kukukanganya kuhusu Mungu, au kukufanya umjaribu Mungu, na isitoshe ili kukupa shaka kuhusu utambulisho na hali halisi ya Mungu. Badala yake, Ninafanya hivi ili kuhimiza ndani yenu ufahamu mkubwa zaidi wa hali halisi ya Mungu, na uhakika na imani kubwa zaidi kuhusu hadhi ya Mungu, ili Mungu awe Ndiye wa pekee katika mioyo ya wale wote wanaomfuata Mungu, na ili ile hadhi ya asili ya Mungu—kama Muumba, Kiongozi wa viumbe vyote, Mungu Mwenyewe wa kipekee—iweze kurejeshwa katika mioyo ya kila kiumbe. Hii pia ndiyo mada itakayohusu ushirika wetu.

Sasa, hebu na tuanze kusoma maandiko yafuatayo kutoka kwenye Biblia.

1. Mungu Hutumia Maneno ili Kuumba Viumbe Vyote

Mwa 1:3-5 Na Mungu akasema, Na kuwe na mwanga; kukawa na mwanga. Mungu akauona mwanga, na kuwa ulikuwa mzuri: na Mungu akautenga mwanga na kiza. Naye Mungu akauita mwanga Mchana, na kiza akaliita Usiku. Na jioni na asubuhi yalikuwa siku ya kwanza.

Mwa 1:6-7 Na Mungu alisema, Na kuwe na mbingu katikati ya maji, na uigawanye maji kutoka kwa maji. Na Mungu akaitengeneza mbingu, na akayagawanya yale maji yaliyokuwa chini ya mbingu kutoka kwa yale maji yaliyokuwa juu ya mbingu: na kukawa vivyo hivyo.

Mwa 1:9-11 Naye Mungu akasema, Nayo maji yaliyo chini ya mbingu yakonge pahali pamoja, na ardhi kavu ionekane; na kukawa vivyo hivyo. Naye Mungu akaiita nchi kavu Dunia: na kukonga kwa maji akakuita Bahari: naye Mungu akaona kwamba ni vyema. Naye Mungu akasema, Na dunia ize majani, mche ambao unatoa mbegu, na mti wa matunda ambao unazaa tunda kwa aina yake, ambao mbegu zake ziko ndani yake, juu ya dunia: na kukawa vivyo hivyo.

Mwa 1:14-15 Naye Mungu akasema, Kuwe na mwangaza katika anga la mbingu kwa minajili ya kutenga mchana na usiku; na uwe ndio ishara; na majira, na siku na miaka: Na tena uwe ndio mwangaza katika anga la mbingu kwa minajili ya kupa nchi nuru; na ikawa vile.

Mwa 1:20-21 Na Mungu akasema, Na maji yalete kwa wingi kiumbe asongaye aliye na uhai, na ndege wanaoweza kuruka juu ya nchi katika anga wazi la mbingu. Naye Mungu

akaumba nyangumi wakubwa, na viumbe wote walio na uhai wasongao, ambao maji yalileta kwa wingi, kwa aina yao, na kila ndege anayeruka kwa aina yake: na Mungu akaona kuwa ilikuwa vizuri.

Mwa 1:24-25 Naye Mungu akasema, Dunia na ilete kiumbe kilicho hai kwa namna yake, mifugo, na kitu kinachotambaa, na wanyama wa mbituni kwa namna yake: na ikafanyika. Naye Mungu akaumba wanyawa wa mbituni kwa namna yake, na mifugo kwa namna yake, na chote kinachotambaa duniani kwa namna yake: na Mungu akaona kwamba ni vizuri.

Kwenye Siku ya Kwanza, Mchana na Usiku wa Mwanadamu Vinazaliwa na Kujitokeza Waziwazi kwa Msaada wa Mamlaka ya Mungu

Hebu na tuweze kuangalia fungu la kwanza: “Na Mungu akasema, Na kuwe na mwanga; kukawa na mwanga. Mungu akauona mwanga, na kuwa ulikuwa mzuri: na Mungu akautenga mwanga na kiza. Naye Mungu akauita mwanga Mchana, na kiza akaliita Usiku. Na jioni na asubuhi yalikuwa siku ya kwanza” (Mwa 1:3-5). Fungu hili linafafanua kitendo cha kwanza cha Mungu wakati wa mwanzo wa uumbaji, na siku ya kwanza ambayo Mungu alipitisha ambapo kulikuwa na jioni na asubuhi. Lakini ilikuwa siku ya kipekee: Mungu alianza kutayarisha nuru ya viumbe vyote, na, vilevile, Akagawa nuru kutoka kwa giza. Kwenye siku hii, Mungu alianza kunena, na matamshi na mamlaka Yake vyote vilikuwa pamoja. Mamlaka Yake yalianza kujitokeza miongoni mwa viumbe vyote, na nguvu Zake zikaenea miongoni mwa viumbe vyote kutokana na maneno Yake. Kuanzia siku hii kuendelea mbele, viumbe vyote viliumbwa na vikawa viko tayari kwa sababu ya maneno ya Mungu, mamlaka ya Mungu na nguvu za Mungu, na vikaanza kufanya kazi kwa msaada wa maneno ya Mungu, mamlaka ya Mungu na nguvu za Mungu. Wakati Mungu aliposema maneno haya “Na kuwe na mwanga,” kulikuwepo na nuru. Mungu hakuanza kushughulikia shughuli yoyote; nuru ilikuwa imeonekana kama matokeo ya maneno Yake. Hii ilikuwa nuru ambayo Mungu aliita mchana, na ambayo binadamu angali anaitegemea kwa minajili ya kuwepo kwake leo. Kwa amri ya Mungu, hali yake halisi na thamani havijawahi kubadilika na havijawahi kutoweka. Uwepo wake unaonyesha mamlaka na nguvu za Mungu, na unatangaza uwepo wa Mungu, na unathibitisha, tena na tena, utambulisho na hadhi ya Muumba. Haiwezi kushikika, au kuonekana, lakini ni nuru halisi inayoweza kuonekana na binadamu. Kuanzia wakati huo kusonga mbele, kwenye ulimwengu huu mtupu ambao “nchi ilikuwa ya ukiwa na tupu; na kulikuwa na giza sehemu ya juu ya vilindi,” kulikuwepo kiumbe kile cha kwanza cha kushikika. Kiumbe hiki kilitokana na maneno ya kinywa cha Mungu na kikaonekana kwenye tukio la kwanza la kuumbwa kwa viumbe vyote kwa sababu ya mamlaka na matamshi ya Mungu. Muda mfupi baadaye, Mungu aliamuru nuru na giza kutengana.... Kila kitu kilibadilika na kilikamilishwa kwa sababu ya maneno ya Mungu....

Mungu akaiita nuru hii “Mchana,” na giza hili Akaliita “Usiku.” Kuanzia wakati huo, jioni ya kwanza na asubuhi ya kwanza ziliweza kuumbwa katika ulimwengu ambao Mungu alinuia kuumba, na Mungu akasema hii ndiyo iliyokuwa siku ya kwanza. Siku hii ilikuwa siku ya kwanza ya vile vilivyoundwa na Muumba wa viumbe vyote, na ilikuwa mwanzo wa kuumbwa kwa viumbe vyote, na ndio wakati wa kwanza ambao mamlaka na nguvu za Muumba vilikuwa vimeonyeshwa katika ulimwengu huu ambao Alikuwa ameumba.

Kupitia maneno haya, binadamu anaweza kutazama mamlaka ya Mungu, na mamlaka ya maneno ya Mungu, na nguvu za Mungu. Kwa sababu Mungu tu ndiye anayemiliki nguvu kama hizo, na kwa hivyo Mungu pekee ndiye aliye na mamlaka, na kwa sababu Mungu ndiye anayemiliki mamlaka kama hayo, kwa hivyo Mungu pekee ndiye aliye na nguvu kama hizo. Je, binadamu au kifaa chochote kingeweza kumiliki mamlaka na nguvu kama hizi? Je, kunalo jibu katika moyo wako? Mbali na Mungu, je, kuna kiumbe chochote kilichoundwa au kile ambacho hakikuumbwa kinachomiliki mamlaka kama hayo? Umewahi kuona mfano wa kiumbe kama hiki kwenye vitabu vingine vyovyote au machapisho? Kunayo rekodi yoyote kwamba mtu aliumba mbingu na ulimwengu na viumbe vyote? Jambo hili halionekani katika vitabu au rekodi nyingine zozote; haya ndiyo, bila shaka, maneno ya kipekee yenye mamlaka na nguvu kuhusu uumbaji wa kupendeza wa Mungu wa ulimwengu, yaliyorekodiwa kwenye Biblia, na maneno haya yanazungumzia mamlaka ya kipekee ya Mungu, na utambulisho wa kipekee wa Mungu. Je, mamlaka na nguvu kama hizi zinaweza kusemekana kuwa zinaashiria utambulisho wa kipekee wa Mungu? Yanaweza kusemwa yanamilikiwa na Mungu, na Mungu pekee? Bila shaka, Mungu Mwenyewe pekee ndiye anayemiliki mamlaka na nguvu kama hizi! Mamlaka na nguvu hizi vyote haviwezi kumilikiwa au kubadilishwa na kiumbe chochote kingine kilichoundwa au kile ambacho hakikuumbwa! Je, hii ni mojawapo ya sifa za Mungu Mwenyewe wa kipekee? Je, umewahi kuishuhudia? Maneno haya yanaruhusu watu kuelewa kwa haraka na waziwazi hoja hii kwamba Mungu anamiliki mamlaka ya kipekee, na nguvu za kipekee, na Anamiliki utambulisho na hadhi isiyo ya kawaida. Kutokana na ushirika wa hapa juu, je, unaweza kusema kwamba Mungu unayemsadiki ndiye Mungu Mwenyewe wa kipekee?

Kwenye Siku ya Pili, Mamlaka ya Mungu Yalipangilia Maji, na Kufanya Mbingu, na Anga za Mbinu za Kimsingi Zaidi za Kuishi kwa Binadamu Kuonekana

Hebu na tusome fungu la pili la Biblia: “Na Mungu alisema, Na kuwe na mbingu katikati ya maji, na uigawanye maji kutoka kwa maji. Na Mungu akaitengeneza mbingu, na akayagawanya yale maji yaliyokuwa chini ya mbingu kutoka kwa yale maji yaliyokuwa juu ya mbingu: na kukawa vivyo hivyo” (Mwa 1:6-7). Ni mabadiliko gani yaliyofanyika baada ya Mungu kusema “Na kuwe na mbingu katikati ya maji, na uigawanye maji kutoka kwa maji”? Maandiko

yanasema: “Na Mungu akaitengeneza mbingu, na akayagawanya yale maji yaliyokuwa chini ya mbingu kutoka kwa yale maji yaliyokuwa juu ya mbingu.” Ni nini kilichokuwa matokeo baada ya Mungu kutamka hivi na kufanya hivyo? Jibu linapatikana kwenye sehemu ya mwisho ya fungu hili: “na kukawa vivyo hivyo.”

Sentensi hizi fupi mbili zinarekodi tukio la kupendeza, na zinafafanua mazingira mazuri— utekelezaji wa kipekee ambapo Mungu aliyatawala maji, na kuunda anga ambayo binadamu angeishi ...

Katika picha hii, maji na anga vinaonekana mbele ya macho ya Mungu papo hapo, na vyote vinagawanywa kwa mamlaka ya matamshi ya Mungu, na kugawanywa kwa sehemu ya juu na ya chini kwa njia ambayo iliteuliwa na Mungu. Hivi ni kusema, anga iliyumbwa na Mungu haikufunika tu maji yaliyo chini, lakini pia ilishikilia maji yaliyo juu.... Katika haya, binadamu hawezi kufanya chochote ila kukodoa macho, kushangaa, na kutweta kwa kuvutiwa na maajabu ya onyesho hilo ambalo Muumba aliyahamisha maji, na kuyaamuru maji, na kuumba anga, na yote haya Alifanya kupitia kwa nguvu za mamlaka Yake. Kupitia kwa matamshi ya Mungu, na nguvu za Mungu, na mamlaka ya Mungu, Mungu aliweza kutimiza tendo jingine kubwa. Je, hizi si nguvu za mamlaka ya Muumba? Hebu na tutumie maandiko haya katika kufafanua vitendo vya Mungu: Mungu aliyatamka matamshi Yake na kwa sababu ya matamshi haya ya Mungu kulikuwa na anga katikati ya maji. Wakati uo huo, badiliko la ajabu lilitokea kwenye nafasi hii kwa sababu ya matamshi haya ya Mungu, na halikuwa badiliko katika hali ya kawaida, lakini aina fulani ya kabadala ambapo kitu kisichokuwepo kiligeuka na kuwa kitu kilichopo. Yote haya yalizaliwa kwenye fikira za Muumba, na yakawa kitu kilichopo kutoka kwenye kitu kisichokuwepo kwa sababu ya matamshi yaliyotamkwa na Muumba, na, vilevile, kuanzia sasa kwenda mbele yangukwepo na kuwa imara, kwa minajili ya Muumba, na yangesonga, kubadilika, na kupata nguvu kulingana na fikira za Muumba. Ufahamu huu unafafanua kitendo cha pili cha Muumba katika viumbe Vyake vya ulimwengu mzima. Yalikuwa maonyesho mengine ya mamlaka na nguvu za Muumba, na ulikuwa utekelezaji mwingine anzilishi uliofanywa na Muumba. Siku hii ndiyo iliyokuwa siku ya pili ambayo Muumba alikuwa amepitisha tangu kuwekwa msingi kwa ulimwengu, na ilikuwa siku nyingine nzuri Kwake: Alitembea miongoni mwa nuru, Aliileta anga, Aliyapangilia na kuyatawala maji, na vitendo Vyake, mamlaka Yake, na nguvu Zake vyote viliweza kuanza kazi kwenye siku hiyo mpya ...

Je, kulikuwepo na anga katikati ya maji kabla ya Mungu kutamka matamshi Yake? Bila shaka la! Na je, baada ya Mungu kusema “Na kuwe na mbingu katikati ya maji”? Viumbe vilivyonuiwa na Mungu vilionekana; kulikuwa na anga katikati ya maji, na maji yaligawanywa kwa sababu Mungu alisema hivyo “na uigawanye maji kutoka kwa maji.” Kwa njia hii, kufuatia

maneno ya Mungu, viumbe vipya viwili, viumbe viwili vilivyozaliwa na vilivyokuwa vipya vilionekana miongoni mwa viumbe vyote kutokana na mamlaka na nguvu za Mungu. Na unahisi vipi kuhusu kujitokeza kwa viumbe hivi viwili vipya? Je, unahisi ukubwa wa nguvu za Muumba? Unahisi ile nguvu ya kipekee na isiyo ya kawaida ya Muumba? Ukubwa wa msukumo na nguvu kama hizo unatokana na mamlaka ya Mungu na mamlaka haya ni kiwakilishi cha Mungu Mwenyewe, na sifa ya kipekee ya Mungu Mwenyewe.

Je, ufahamu huu umekupa mtazamo mwingine kamilifu wa upekee wa Mungu? Lakini haya ni machache tu kati ya mengi; mamlaka na nguvu za Muumba vinazidi haya yote. Upekee wake hauko hivyo tu kwa sababu Anamiliki hali halisi isiyo kama ya viumbe vingine, lakini pia kwa sababu ya mamlaka na nguvu Zake kuwa zisizo za kawaida, zisizo na mipaka, bora kabisa kuliko vyote, na inapita vitu vyote, na vilevile, kwa sababu mamlaka Yake na kile Anacho na alichokinaaweza kuumba maisha, na kufanya miujiza, na Anaweza kuumba kila mojawapo ya dakika na sekunde iliyo ya kustaajabisha na isiyo ya kawaida, na wakati uo huo, Anaweza kutawala maisha Anayoyaumba na kushikilia ukuu Wake juu ya miujiza na kila mojawapo ya dakika na sekunde Anazoumba.

Kwenye Siku ya Tatu, Matamshi ya Mungu Yazaa Ardhi na Bahari, na Mamlaka ya Mungu Yasababisha Ulimwengu Kujaa Maisha

Sasa, hebu na tusome sentensi ya kwanza ya Mwanzo 1:9-11: “Naye Mungu akasema, Nayo maji yaliyo chini ya mbingu yakonge pahali pamoja, na ardhi kavu ionekane.” Ni mabadiliko gani yaliyotokea baada ya Mungu kusema tu, “Nayo maji yaliyo chini ya mbingu yakonge pahali pamoja, na ardhi kavu ionekane”? Na hii nafasi iliyokuwa katikati ya nuru na anga ilikuwa nini? Katika Maandiko, imeandikwa: “Naye Mungu akaiita nchi kavu Dunia: na kukonga kwa maji akakuita Bahari: naye Mungu akaona kwamba ni vyema.” Hivi ni kusema, kulikuwepo sasa na ardhi na bahari kwenye anga hii, nayo ardhi na bahari viliweza kutenganishwa. Kujitokeza kwa vitu hivi vipya kulifuata amri kutoka kwenye kinywa cha Mungu, “na kukawa vivyo hivyo.” Je, Maandiko yanafafanua Mungu akiwa ameshughulika kila pahali wakati Akifanya haya? Je, yanafafanua Mungu akiwa anajihusisha katika kazi ngumu? Kwa hivyo, haya yote yaliwezaje kufanywa na Mungu? Mungu aliwezaje kusababisha vitu hivi vipya kuumbwa? Tunaelewa wenyewe bila kuelezewa, kwamba Mungu alitumia matamshi kutimiza mambo haya yote, kuumba uzima wa haya yote.

Kwenye mafungu matatu yaliyo hapo juu, tumejifunza kunatokea matukio matatu makubwa. Matukio haya matatu makubwa yalionekana, na yakaumbwa kuwa hivyo, kupitia kwa matamshi ya Mungu, na ni kwa sababu ya matamshi Yake ndipo, moja baada ya lingine, yaliweza kujitokeza mbele ya macho ya Mungu. Kwa hivyo inaweza kuonekana kwamba

“Mungu huongea, na ikatimizwa; huamuru, na ikawa imara” haya si maneno matupu. Hali hii halisi ya Mungu inathibitishwa wakati ule ambao fikira Zake zinaeleweka, na wakati ambapo Mungu hufungua kinywa Chake kuongea, hali Yake halisi inajionyesha kikamilifu.

Hebu na tuendeleo hadi kwenye sentensi ya mwisho ya fungu hili: “Naye Mungu akasema, Na dunia ize majani, mche ambao unatoa mbegu, na mti wa matunda ambao unazaa tunda kwa aina yake, ambao mbegu zake ziko ndani yake, juu ya dunia: na kukawa vivyo hivyo.” Huku Mungu akiongea, mambo haya yote yaliumbika kufuatia fikira za Mungu, na kwa muda mfupi tu, mseto wa viumbe vidogo vinyonge vyenye maisha vilikuwa vinachomoza vichwa vyao kwa kusita huku vichwa vyao vikiwa juu kupitia kwenye ardhi, na hata kabla ya kukung’uta chembechembe za uchafu kutoka kwenye miili yao vilikuwa vikipungiana mikono kusalimiana kwa hamu, kuitikia na kuufurahia ulimwengu. Vilishukuru Muumba kwa maisha aliyovipatia, na kuutangazia ulimwengu kwamba vilikuwa sehemu ya viumbe vyote, na kwamba kila kimojawapo kingejitolea katika maisha yavyo ili viwe vinaonyesha mamlaka ya Muumba. Kama vile matamshi ya Mungu yalivyotamkwa, ardhi ikawa yenye rutuba na kijani, aina zote za miti ambayo ingeweza kufurahiwa na binadamu iliweza kuota na kuchipuka kutoka kwenye ardhi, na milima na nchi tambarare vyote vikawa na idadi kubwa ya miti na misitu.... Ulimwengu huu tasa, ambao hakukuwahi kuwepo na chembechembe zozote za maisha, ulifunikwa mara moja na wingi wa nyasi, mimea ya msimu na miti na ilikuwa ikifurika kwa kijani kibichi kingi.... Harufu nzuri ya nyasi na mnukio wa mchanga uliosambazwa kupitia hewani, na mseto wa mimea vyote vilianza kupumua kulingana na mzunguko wa hewa, na vikaanza pia mchakato wa kukua. Wakati uo huo, kutokana na maneno ya Mungu na kufuatia fikira za Mungu, mimea yote ilianza mizunguko isiyoisha ya maisha ambapo inakua, inanawiri, inazaa matunda na kuzaana na kuongezeka. Ilianza kutii kwa umakinifu mikondo yao husika ya maisha na kuanza kutekeleza wajibu wao husika miongoni mwa viumbe vyote.... Yote ilizaliwa na kuishi, kwa sababu ya matamshi ya Muumba. Ingepokea matoleo na ustawishaji usiosita wa Muumba, na siku zote ingeendelea kuishi kwa shauku katika kila pembe ya ardhi ili kuonyesha mamlaka na nguvu za Muumba, na siku zote ingeonyesha nguvu za maisha walizopewa na Muumba ...

Maisha ya Muumba ni yale yasiyo ya kawaida, fikira Zake ni zile zisizo za kawaida, na mamlaka Yake ni yale yasiyokuwa ya kawaida, na kwa hivyo, wakati matamshi Yake yalipotamkwa, yale matokeo ya mwisho yalikuwa “na ikawa hivyo.” Ni wazi kwamba, Mungu hahitaji kufanya kazi kwa mikono Yake wakati Anapofanya matendo; Anatumia tu fikira Zake kutoa amri, na matamshi Yake ili kuagizia, na kwa njia hii mambo yanatimizwa. Kwenye siku hii, Mungu aliyakusanya maji katika mahali pamoja, na Akaiacha ardhi kavu kujitokeza, baada ya hapo Mungu aliifanya nyasi kuota kutoka kwenye ardhi, na papo hapo palimea mimea ya msimu iliyozaa mbegu, na miti ya kuzaa matunda, na Mungu akaainisha kila mojawapo

kulingana na aina, na kusababisha kila mmea kuwa na mbegu yake. Haya yote yaliwezekana kulingana na fikira za Mungu na amri za matamshi ya Mungu, na kila mmea ulijitokeza, mmoja baada ya mwingine, kwenye ulimwengu huu mpya.

Wakati Alikuwa aanze kazi Yake, Mungu tayari alikuwa na picha ya kile Alichonuia kutimiza katika akili Zake na wakati ambapo Mungu alianza kutimiza mambo haya, na ndio wakati ambao pia Mungu alikifungua kinywa Chake kuongea kuhusu maudhui ya picha hii, mabadiliko katika viumbe vyote yalianza kufanyika kutokana na mamlaka na nguvu za Mungu. Bila ya kujali namna Mungu alivyofanya, au namna Alivyoonyesha mamlaka Yake, kila kitu kilitimizwa hatua kwa hatua kulingana na mpango wa Mungu na kwa sababu ya matamshi ya Mungu, na mabadiliko ya hatua kwa hatua yalifanyika kati ya mbingu na ardhi kutokana na matamshi na mamlaka ya Mungu. Mabadiliko na matukio haya yote yalionyesha mamlaka ya Muumba, na nguvu za maisha ya Muumba zisizo za kawaida na zenye ukubwa. Fikira Zake si mawazo mepesi, au picha tupu, lakini mamlaka yanayomiliki nishati kuu na ile isiyo ya kawaida, na ndio nguvu zinazosababisha viumbe vyote kubadilika, kufufua, kupata nguvu upya, na kuangamia. Kwa sababu ya haya, viumbe vyote hufanya kazi kwa sababu ya fikira Zake, na, wakati uo huo, yote haya yanatimizwa kwa sababu ya matamshi kutoka kinywa Chake ...

Kabla ya viumbe vyote kujitokeza, kwenye akili za Mungu mpango wa Mungu ulikuwa umeundwa kitambo, na ulimwengu mpya ulikuwa umetimizwa kitambo. Ingawa kwenye siku ya tatu mmea aina yote ilijitokeza ardhini, Mungu hakuwa na sababu yoyote ya kusitisha hatua za uumbaji Wake kwa ulimwengu huu, Alinuia kuendelea kunena matamshi Yake, kuendelea kutimiza uumbaji wa kila kiumbe kipya. Angenena, angetoa amri Zake, na angeonyesha mamlaka Yake na kuendeleza nguvu Zake, na Alitayarisha kila kitu Alichokuwa amepanga ili kutayarishia viumbe vyote na mwanadamu ambaye Alinuia kuumba ...

Kwenye Siku ya Nne, Misimu, Siku, na Miaka ya Mwanadamu Iliumbika Huku Mungu Akionyesha Mamlaka Yake kwa Mara Nyingine Tena

Muumba alitumia matamshi Yake kutimiza mpango Wake, na kwa njia hii Alipitisha siku tatu zake za kwanza kwenye mpango Wake. Kwenye siku hizi tatu, Mungu hakuonekana kushughulika kila pahali, au kujichosha Yeye Mwenyewe; kinyume cha mambo ni kwamba, Alikuwa na siku tatu za kwanza nzuri katika mpango Wake na Alitimiza utekelezaji mkubwa wa mabadiliko makubwa ya ulimwengu. Ulimwengu mpya kabisa ulijitokeza mbele ya macho Yake, na, kipande kwa kipande, picha nzuri na ya kupendeza ambayo ilikuwa imefichwa ndani ya fikira Zake ilikuwa tayari imefichuliwa kwa matamshi ya Mungu. Kujitokeza kwa kila kiumbe kipya kulikuwa sawa na kuzaliwa kwa mtoto mchanga, na Muumba alifurahia sana picha hii ambayo iliwahi kuwa kwenye fikira Zake, lakini ambayo sasa ilikuwa imepewa uhai. Wakati

huu, moyo Wake ulifaidi sehemu ndogo ya kutosheka, lakini mpango Wake ulikuwa ndio tu umeanza. Punde si punde, siku mpya ilikuwa imewadia—na ukurasa unaofuata ulikuwa upi kwenye mpango wa Muumba? Ni nini Alichosema? Na Aliwezaje kuonyesha mamlaka Yake? Na, wakati uo huo, ni mambo yapi mapya yaliyokuja kwenye ulimwengu huu mpya? Kufuatia mwongozo wa Muumba, kuangaza kwetu kwa macho kunatufikisha kwenye siku ya nne ya uumbaji wa Mungu wa viumbe vyote, siku ambayo ilikuwa ni mwanzo mpya. Bila shaka, kwa Muumba, bila tashwishi ilikuwa ni siku nyingine nzuri, na siku nyingine yenye umuhimu mkubwa kwa mwanadamu wa leo. Ilikuwa, bila shaka, siku yenye thamani isiyopimika. Ilikuwaje nzuri, ilikuwaje muhimu, na ilikuwaje yenye thamani isiyopimika? Hebu na tuweze kusikiliza matamshi yaliyotamkwa na Muumba....

“Naye Mungu akasema, Kuwe na mwangaza katika anga la mbingu kwa minajili ya kutenga mchana na usiku; na uwe ndio ishara; na majira, na siku na miaka: Na tena uwe ndio mwangaza katika anga la mbingu kwa minajili ya kupa nchi nuru; na ikawa vile” (Mwa 1:14-15). Haya yalikuwa maonyesho mengine ya mamlaka ya Mungu yaliyoonyeshwa kwa viumbe kufuatia uumbaji Wake wa ardhi kavu na mimea iliyokuwa juu yake. Kwa Mungu, kitendo kama hicho kilikuwa tu rahisi kama kile Alichokuwa tayari Amefanya, kwa sababu Mungu ana nguvu kama hizo; Mungu ni mzuri kama vile tu neno Lake lilivyo, na neno Lake litatimizwa. Mungu aliamuru nuru kujitokeza mbinguni, na nuru hizi hazikuangaza tu kwenye mbingu lakini pia kwenye ardhi, lakini pia zilihudumu kama ishara za mchana na usiku, kwa minajili ya misimu, siku, na miaka. Kwa njia hii, kama vile Mungu alivyoongea kwa matamshi Yake, kila kitendo ambacho Mungu alipenda kutimiza kilitimizwa kulingana na maana ya Mungu na kwa njia iliyoteuliwa na Mungu.

Nuru kwenye mbingu ni viumbe vilivyo kwenye mbingu vinavyoweza kuonyesha nuru; vinaweza kuangazia mbingu, na vinaweza kuangazia ardhi na bahari. Vinazunguka kulingana na mpigo na mara ngapi ambapo vimeamriwa na Mungu, na vinaangaza sehemu mbalimbali zenye vipindi tofauti vya muda kwenye ardhi, na kwa njia hii mizunguko ya kuzunguka kwa nuru hizi husababisha mchana na usiku kujitokeza upande wa mashariki na magharibi mwa ardhi, na wala si tu ishara za usiku na mchana, lakini kupitia kwa mizunguko hii tofauti inaweza kuadhimisha pia karamu na siku mbalimbali maalum za mwanadamu. Ndizo nyongeza na saidizi timilifu kwa misimu minne—mchipuko, kiangazi, mapukutiko, na kipupwe—iliyotolewa na Mungu, pamoja na vile ambavyo nuru hizi huhudumu kwa mpangilio maalum kama alama za mara kwa mara na sahihi kwa minajili ya vipimo mbalimbali, siku, na miaka ya mwanadamu. Ingawa ilikuwa baada tu ya mwanzo wa kilimo ndipo mwanadamu alipoanza kuelewa na kukumbana na utofautishaji wa vipimo vya muda, siku, na miaka iliyosababishwa na nuru hizi zilizoumbwa na Mungu, kwa hakika, vipindi vya muda, siku, na miaka ambavyo binadamu anaelewa leo vilianza kutolewa

kitambo kwenye siku ya nne ya uumbaji wa viumbe vyote na Mungu, na vilevile ndivyo ilivyokuwa kwenye mizunguko inayobadilishana ya mchipuko, kiangazi, mapukutiko, na kipupwe ambavyo binadamu anapitia na vinaanza kitambo kwenye siku ya nne ya uumbaji wa Mungu wa vitu vyote. Nuru zile zilizoumbwa na Mungu zilimwezesha binadamu kuweza kutofautisha mara kwa mara, kwa hakika, na waziwazi usiku na mchana, na kuhesabu siku, na kuweza kufuatilia waziwazi vipindi vile vya muda na miaka. (Siku ya mwezi mzima ilikuwa kukamilika kwa mwezi mmoja, na kutokana na haya binadamu alijua kwamba kule kuangazia kwa nuru kulianzisha mzunguko mpya; siku ile ya nusu mwezi ilikuwa ni kukamilika kwa nusu moja ya mwezi, jambo ambalo lilimfahamisha binadamu kwamba kipindi kipa cha muda kilikuwa kimeanza, ambapo binadamu angeweza kujua ni mchana na usiku ngapi vilikuwa kwenye kipindi cha muda, na ni vipindi vingapi vya muda vilikuwa kwenye msimu, na ni misimu mingapi ilikuwa kwenye mwaka, na vyote hivi vilionyeshwa mara kwa mara.) Kwa hivyo, binadamu angeweza kufuatilia kwa urahisi vipindi vya muda, siku, na miaka iliyowekewa alama na mizunguko ya nuru hizo. Kuanzia sasa kusonga mbele, mwanadamu na viumbe vyote viliishi bila kufahamu miongoni mwa mabadiliko yenye mpangilio ya usiku na mchana na kubadilishwa kwa misimu iliyotokana na mizunguko ya nuru. Huu ndio ulikuwa muhimu wa uumbaji wa Muumba wa nuru kwenye siku ya nne. Vilevile, nia na umuhimu wa hatua hii ya Muumba vilikuwa bado haviwezi kutenganishwa na mamlaka na nguvu Zake. Na kwa hivyo, nuru zilizoumbwa na Mungu na thamani ambayo zingeleta hivi karibuni kwa binadamu ilikuwa ni mafanikio mengine katika uonyeshaji wa mamlaka ya Muumba.

Katika ulimwengu huu mpya, ambao mwanadamu bado alikuwa hajaonekana, Muumba alikuwa ametayarisha jioni na asubuhi, ile anga, ardhi na bahari, nyasi, miti isiyozaa na aina mbalimbali za miti, na nuru, misimu, siku, na miaka kwa minajili ya maisha mapya ambayo Angeumba hivi karibuni. Mamlaka na nguvu za Muumba vyote vilionyeshwa katika kila kiumbe kipa Alichokiumba, na maneno na kufanikiwa Kwake vyote vilifanyika sawia, bila ya hitilafu yoyote ndogo na bila ya kuchelewa kokote kudogo. Kujitokeza na kuzaliwa kwa viumbe hivi vyote vipya kulikuwa ithibati ya mamlaka na nguvu za Muumba: Yeye ni mzuri sawa tu na neno Lake, na neno Lake litakamilika, na kile kinachokamilika kinadumu milele. Hoja hii haijawahi kubadilika: ndivyo ilivyokuwa kale, ndivyo ilivyo leo, na ndivyo itakavyokuwa daima dawamu. Unapoyaangalia kwa mara nyingine maneno hayo ya maandiko, unahisi kwamba yangali mapya kwako? Je, umeyaona maudhui mapya, na kufanya ugunduzi mpya? Hii ni kwa sababu vitendo vya Muumba vimechangamsha moyo wako na kuongoza mwelekeo wa maarifa yako ya mamlaka na nguvu Zake, na yakakufungulia mlango wa ufahamu wa Muumba, na vitendo na mamlaka Yake vimeweza kupatia maneno haya uhai. Na kwa hivyo katika maneno haya binadamu ameona maonyesho halisi, na wazi ya mamlaka ya Muumba, na kuweza kushuhudia

kwa kweli mamlaka makuu ya Muumba, na kutazama mamlaka yake yasiyokuwa ya kawaida na nguvu za Muumba.

Mamlaka na nguvu za Muumba hutoa muujiza baada ya muujiza na huvutia umakinifu wa binadamu, naye binadamu hawezi kukwepa haya ila kuyaangazia tu macho matendo haya ya kipekee yaliyozaliwa kutokana na utekelezaji wa mamlaka husika. Nguvu zake za kipekee zafurahisha baada ya kufurahisha, na binadamu anabaki akishangaa na akijawa na furaha, naye anatweta kwa kuvutiwa, anastaajabishwa, na kushangilia; nini kingine tena, binadamu amefurahishwa kwa kumtazama alivyo, na kilichozaliwa ndani yake ni heshima, kustahi, na mtagusano wa karibu. Mamlaka na vitendo vya Muumba vinayo athari kwa roho ya binadamu na hutakasa roho ya binadamu na zaidi, kutosheleza roho ya binadamu. Kila mojawapo ya fikira Zake, kila mojawapo ya matamshi Yake, na kila ufunuo wa mamlaka Yake ni kiungo muhimu miongoni mwa viumbe vyote, na ni utekelezaji mkuu wenye thamani zaidi wa kuunda ufahamu na maarifa ya kina ya mwanadamu. Tunapohesabu kila kiumbe kilichozaliwa kutokana na matamshi ya Muumba, roho zetu zinavutiwa kwa maajabu ya nguvu za Mungu, na tunajipata tukifuata nyayo za Muumba hadi kwenye siku inayofuata: siku ya tano ya uumbaji wa Mungu wa viumbe vyote.

Hebu tuendeleo kusoma Maandiko fungu hadi fungu, tunapoangalia vitendo vingi zaidi vya Muumba.

Kwenye Siku ya Tano, Maisha ya Maumbo Tofauti na Pana Yaonyesha Mamlaka ya Muumba kwa Njia Tofauti

Maandiko yanasema, “Na Mungu akasema, Na maji yalete kwa wingi kiumbe asongaye aliye na uhai, na ndege wanaoweza kuruka juu ya nchi katika anga wazi la mbingu. Naye Mungu akaumba nyangumi wakubwa, na viumbe wote walio na uhai wasongao, ambao maji yalileta kwa wingi, kwa aina yao, na kila ndege anayeruka kwa aina yake: na Mungu akaona kuwa ilikuwa vizuri” (Mwa 1:20-21). Maandiko yanatwambia waziwazi kwamba, kwenye siku hii, Mungu aliumba viumbe vya majini na ndege wa hewani, hivi ni kusema kwamba Aliwaumba samaki na ndege mbalimbali, na akawaainisha kila mmoja wao kulingana na aina. Kwa njia hii, ardhi, mbingu, na maji vyote vilitajirishwa na uumbaji wa Mungu ...

Kama vile maneno ya Mungu yalivyotamkwa, maisha mapya mazuri, kila mojawapo ikiwa na umbo tofauti, kwa ghafla vilipata uhai miongoni mwa matamshi ya Muumba. Viliingia ulimwenguni vikijitikisatikisa kwa minajili ya kupata nafasi, kuruka, kurukaruka kwa furaha.... Samaki wa maumbo na ukubwa wote waliweza kuogelea majini; samakigamba wa kila aina waliweza kukua kwenye michanga, viumbe vyenye magamba, vyenye maganda na vile

visivyokuwa na uti wa mgongo viliweza kukua kwa haraka kwa maumbo tofauti, haijalishi kama vilikuwa vikubwa au vidogo, virefu au vifupi. Na ndivyo pia ilivyokuwa kwa aina tofauti za mwani kuanza kukua kwa haraka, ikiyumbayumba kutokana na msongo wa maisha mbalimbali ya majini, yasiyosita, na yanayosihi yale maji tulivu, ni kana kwamba yanataka kuyaambia: Tikisa mguu! Walete marafiki wako! Kwani hutawahi kuwa pekee tena! Kuanzia muda ule ambao viumbe mbalimbali vilivyo na uhai viliumbwa na Mungu na kuonekana majini, kila maisha mapya yalileta nguvu kwenye maji yaliyokuwa tulivu kwa muda mrefu, na kuweza kuanzisha enzi mpya.... Kuanzia hapo kwenda mbele, viumbe hivi viliishi pamoja, kimoja kando ya kingine na vikaweza kutangamana pamoja, na havikuweka umbali kati yao. Yale maji yalikuwepo kwa minajili ya viumbe vilivyokuwa ndani yake, yakipatia uhai kila maisha yaliyokuwa karibu na kumbatio lake, na kila maisha yalikuwepo kwa minajili ya maji kwa sababu ya uhai wake. Kila moja ilipatia uhai mwenzake, na wakati uo huo, kila kimoja, kwa njia hiyo, kilitolea ushuhuda wa miujiza na ukubwa wa uumbaji wa Muumba, na kwa nguvu zisizoshindwa za mamlaka ya Muumba ...

Kwa vile bahari haikuwa tulivu tena, ndivyo pia maisha yalivyoanza kujaza mbingu. Mmoja baada ya mwingine, ndege, wakubwa na wadogo, walipaa kwenye mbingu kutoka ardhini. Tofauti na viumbe vya baharini, walikuwa na mbawa na manyoya ambayo yalifunika maumbo yao membamba na yenye neema. Walipigapiga mbawa zao, kwa maringo na majivuno wakionyesha koti lao la kupendeza la manyoya na kazi zao maalum pamoja na mbinu walizopewa na Muumba. Walipaa kwa uhuru, na kwa mbinu walizokuwa nazo wakapaa katikati ya mbingu na ardhi, kote kote kwenye mbuga na misitu.... Walikuwa ndio wapenzi wa hewani, walikuwa ndio wapenzi wa viumbe vyote. Hivi punde ndio wangekuwa kiunganishi kati ya mbingu na ardhi, na wangepitisha ujumbe kwa viumbe vyote.... Waliimba, wakawa wanapaapaa kwa furaha kote kote, walileta vifijo, vicheko, na uchangamfu kwenye ulimwengu huu uliojaa utupu hapo mwanzoni.... Walitumia kuimba kwao kwa uwazi, kuvutia, na kutumia maneno yaliyokuwa ndani ya mioyo yao kusifu Muumba kwa maisha aliyowapa. Walicheza kwa uchangamfu ili kuonyesha utimilifu na miujiza ya uumbaji wa Muumba, na wangejitolea maisha yao yote kushuhudia agano la mamlaka ya Muumba kupitia kwenye maisha maalum ambayo Alikuwa amewapa ...

Licha ya kama vilikuwa majini, au mbinguni, kwa amri ya Muumba, wingi huu wa viumbe hivi hai ulikuwepo katika mipangilio tofauti ya maisha, na kwa amri ya Muumba, vilikusanyika pamoja kulingana na aina zao mbalimbali—na sheria hii, kanuni hii, ilikuwa isiyoweza kubadilishwa na viumbe vyovyote. Havikuwahi kuthubutu kwenda nje ya mipaka viliyowekewa na Muumba, na wala visingeweza kufanya hivyo. Kama walivyoamriwa na Muumba, waliishi na kuzaana, na kutii kwa umakinifu mkondo wa maisha na sheria walizowekewa na Muumba, na

kwa kufahamu wakafuata amri Zake zisizotamkwa na amri na maagizo ya mbinguni Aliyowapa, kutoka hapo hadi leo. Walizungumza na Muumba kwa njia yao wenyewe maalum, na wakashukuru maana ya Muumba, na wakatii amri Zake. Hakuna kati yao aliyewahi kukiuka mamlaka ya Muumba, na ukuu na amri Yake juu yao ilitekelezwa ndani ya fikira Zake; hakuna maneno yaliyotolewa, lakini mamlaka yaliyokuwa ya kipekee kwa Muumba yalidhibiti viumbe vyote kwa kimya ambacho hakikumiliki matumizi yoyote ya lugha, na iliyokuwa tofauti na mwanadamu. Utiliaji mkazo wa mamlaka Yake kwa njia hii maalum ulimshawishi binadamu kupata maarifa mapya, na kuufanya ufasiri mpya wa mamlaka ya kipekee ya Mungu. Hapa, lazima Niwaambie kwamba kwenye siku hii mpya, ule utiliaji mkazo wa mamlaka ya Muumba ulionyesha kwa mara nyingine ule upekee wa Muumba.

Kinachofuata, wacha tuangalie sentensi ya mwisho ya fungu hili la maandiko: “Mungu akaona kwamba ni vizuri.” Unafikiri hii inamaanisha nini? Hapa, tunapata kuziona hisia za Mungu. Mungu alitazama viumbe vyote Alivyokuwa ameumba vikiumbika na kusimama wima kwa sababu ya matamshi Yake, na kwa utaratibu vikianza kubadilika. Wakati huu, Mungu alikuwa ametosheka na mambo mbalimbali Aliyoyaumba kwa matamshi Yake, na vitendo mbalimbali Alivyokuwa ametimiza? Jibu ni kwamba “Mungu akaona kwamba ni vizuri.” Wewe unaona nini hapa? Kinawakilisha nini kwamba “Mungu akaona kwamba ni vizuri”? Kusema hivi kunaashiria nini? Kunamaanisha kwamba Mungu alikuwa na nguvu na hekima ya kukamilisha kile Alichokuwa amepangilia na kushauri, kukamilisha shabaha Alizokuwa ameweka wazi ili kuzikamilisha. Baada ya Mungu kukamilisha kila kazi, je, Alijutia chochote? Jibu lingali kwamba “Mungu akaona kwamba ni vizuri.” Kwa maneno mengine, Hakujutia chochote, lakini Alitosheka. Ni nini maana ya Yeye kutojutia chochote? Tunaelezewa kwamba Mpango wa Mungu ni mtimilifu, kwamba nguvu na hekima Zake ni timilifu, na hiyo ni kutokana tu na mamlaka Yake kwamba utimilifu kama huo unaweza kukamilishwa. Wakati binadamu anapotekeleza kazi, je, anaweza, kama Mungu, kuona kwamba kazi hiyo ni nzuri? Je, kila kitu anachofanya binadamu kinaweza kukamilika na kuwa timilifu? Je, binadamu anaweza kukamilisha kitu mara moja na kikawa hivyo daima dawamu? Kama vile tu binadamu anavyosema, “hakuna kitu kilicho timilifu, kinaweza tu kuwa bora zaidi,” hakuna kitu ambacho binadamu hufanya kinaweza kufikia utimilifu. Wakati Mungu alipoona kwamba kile Alichokuwa amefanya na kutimiza kilikuwa kizuri, kila kitu kilichoumbwa na Mungu kiliwekwa kwa matamshi Yake, hivi ni kusema kwamba, wakati “Mungu akaona kwamba ni vizuri,” kila kitu Alichoumba kikachukua mfumo wa kudumu, kikaainishwa kulingana na aina, na kikapewa mahali maalum, kusudio, na kazi, kwa mara ya kwanza na kwa daima dawamu. Vilevile, wajibu wao miongoni mwa viumbe vyote na safari ambayo lazima waabiri kwenye usimamizi wa Mungu wa viumbe vyote, ulikuwa tayari umeamriwa na Mungu, na usingebadilishwa. Hii

ilikuwa sheria ya mbinguni iliyotolewa na Muumba kwa viumbe vyote.

“Mungu akaona kwamba ni vizuri,” matamshi haya mepesi, yasiyopongezwa, yanayopuuzwa mara nyingi, ndiyo matamshi ya sheria ya mbinguni na maelekezo ya mbinguni kwa viumbe vyote kutoka kwa Mungu. Ni mfano mwingine halisi wa mamlaka ya Muumba, mfano ambao ni wa kimatendo zaidi na unaojitokeza zaidi. Kupitia kwa matamshi Yake, Muumba hakuweza tu kufaidi kila kitu Alichoweka wazi ili kufaidi, na kutimiza kila kitu Alichoweka wazi ili kutimiza, lakini pia Aliweza kudhibiti mikononi Mwake, kila kitu Alichokuwa ameumba, na kutawala kila kitu Alichokuwa ameumba kulingana na mamlaka Yake, na, vilevile, kila kitu kilikuwa cha mfumo na cha kawaida. Viumbe vyote pia vilizaa, vikawepo na vikaangamia kwa matamshi Yake na, vilevile, kwa mamlaka Yake, vilikuwepo katikati ya sheria Aliyokuwa ameiweka wazi, na hakuna kiumbe kilichoachwa! Sheria hii ilianza punde tu “Mungu alipoona kuwa ni vyema,” na itakuwepo, itaendelea, na kufanya kazi kwa minajili ya mpango wa Mungu wa usimamizi mpaka siku ile itabatilishwa na Muumba! Upekee wa mamlaka ya Muumba ulionyeshwa si tu katika uwezo Wake wa kuumba viumbe vyote na kuamuru viumbe vyote kuwepo, lakini pia katika uwezo Wake wa kutawala na kushikilia ukuu juu ya viumbe vyote, na kupatia maisha na nguvu kwa viumbe vyote, na, vilevile, katika uwezo Wake kusababisha, kwa mara ya kwanza na kwa daima dawamu, viumbe vyote ambavyo Angeumba katika mpango Wake ili kuonekana na kuwepo katika ulimwengu ulioundwa na Yeye kwa umbo timilifu, na kwa muundo wa maisha timilifu, na wajibu timilifu. Na ndivyo pia ilivyoonyeshwa kwa njia ambayo fikira za Muumba hazikutegemea vizuizi vyovyote, hazikuwekewa mipaka ya muda, nafasi, au jiografia. Kama mamlaka Yake, utambulisho wa kipekee wa Muumba utabakia vilevile milele hata milele. Mamlaka yake siku zote yatakuwa uwakilishi na ishara ya utambulisho Wake wa kipekee, na mamlaka Yake yatakuwepo milele sambamba na utambulisho Wake!

Kwenye Siku ya Sita, Muumba Aongea, na Kila Aina ya Kiumbe Hai Akilini Mwake Chajitokeza, Kimoja Baada ya Kingine

Bila kuchoka, kazi ya Muumba ya kuumba viumbe vyote ilikuwa imeendelea kwa siku tano, na punde tu baada ya hapo ndipo Muumba alipokaribisha siku ya sita ya uumbaji Wake wa viumbe vyote. Siku hii ilikuwa mwanzo mwingine mpya, na siku nyingine isiyo ya kawaida. Nini, basi, kilikuwa mpango wa Muumba mkeshwa wa siku hii mpya? Ni viumbe vipi vipya ambavyo Angezalisha, je, Angeviumba? Sikiliza, hii ndiyo sauti ya Muumba ...

“Naye Mungu akasema, Dunia na ilete kiumbe kilicho hai kwa namna yake, mifugo, na kitu kinachotambaa, na wanyama wa mbituni kwa namna yake: na ikafanyika. Naye Mungu akaumba wanyawa wa mbituni kwa namna yake, na mifugo kwa namna yake, na chote

kinachotambaa duniani kwa namna yake: na Mungu akaona kwamba ni vizuri” (Mwa 1:24-25). Viumbe hai gani ndivyo vinavyojumuishwa hapa? Maandiko yanasema: ng’ombe, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake. Hivi ni kusema kwamba, kwenye siku hii hakukuweco tu na aina zote za viumbe hai kwenye nchi, lakini pia vyote vilikuwa vimeainishwa kulingana na aina, na, vilevile, “Mungu akaona ya kuwa ni vizuri.”

Kama tu kwenye siku zile tano za awali, na kwa sauti sawa, kwenye siku ya sita Muumba akashurutisha kuzaliwa kwa viumbe hai Alivyotamani, na vikajitokeza kwenye nchi, kila kimoja kulingana na aina yake. Wakati Muumba anapotekeleza mamlaka Yake, hakuna matamshi Yake yanayotamkwa bure bilashi, na kwa hivyo, kwenye siku ya sita, kila kiumbe hai ambacho Alikuwa amenuia kuumba kikajitokeza wakati ule Aliochagua. Muumba aliposema “Dunia na ilete kiumbe kilicho hai kwa namna yake,” nchi ilijawa mara moja na maisha, na juu ya ardhi kukaibuka pumzi za aina zote za viumbe hai.... Kwenye jangwa lenye nyasi za kijani, ng’ombe wanene, wakichezesha mikia yao huku na kule, walijitokeza mmoja baada ya mwingine, kondoo waliokuwa wakitoa milio walikusanyika kwa makundi, na farasi waliotoa milio wakaanza kurukaruka.... Mara moja, nchi pana tambarare yenye utulivu ikajaa uhai.... Kujitokeza kwa mifugo hii mbalimbali kulikuwa mandhari ya kupendeza kwenye nchi ile tambarare iliyotulia, na kujitokeza huko kukaleta nguvu zisizo na mipaka.... Wangukuwa wenza wa nchi ile tambarare, na wenyeji wakuu wa nchi ile tambarare, kila mmoja akitegemea mwingine; na vilevile ndivyo pia wangukuwa walezi na walinzi wa ardhi hizi, ambazo zingekuwa makao yao ya kudumu, na ambazo zingewapa kila kitu walichohitaji, chanzo cha ukuzwaji wa milele kwa minajili ya kuwepo kwao ...

Kwenye siku iyo hiyo ambayo mifugo hii mbalimbali ilijitokeza, kwa tamko la Muumba, wadudu wengi pia walijitokeza, mmoja baada ya mwingine. Hata Ingawa ndio waliokuwa viumbe hai wadogo zaidi miongoni mwa viumbe vyote, nguvu zao za uhai zilikuwa bado uumbaji wa kimiujiza wa Muumba, na hawakuwasili wakiwa wamechelewa sana.... Baadhi yao walipigapiga mabawa yao madogo, huku wengine wakitambaa polepole; baadhi waliruka juu kwa juu, wengine wakapepesuka; wengine walichimba wakienda mbele, huku wengine wakirudi nyuma kwa haraka; wengine walienda upandeupande, wengine wakaruka juu na chini.... Wote walishughulika kwa kujaribu kujitafutia makao: Baadhi walisukumana na kujipata kwenye nyasi, baadhi walianza kuyachimba mashimo ardhini, baadhi wakapaa hadi kwenye miti, wakiwa wamejificha kwenye msitu.... Ingawa walikuwa wadogo kwa ukubwa, hawakuwa radhi kuvumilia mateso ya njaa, na baada ya kupata makao yao binafsi, walikimbia kutafuta chakula ili kuweza kujilisha. Baadhi yao walipanda juu ya nyasi ili wale ncha zake laini, baadhi yao walikamata uchafu kwenye vinywa vyao na kuanza kulisha matumbo yao, wakila kwa bidii na kwa furaha (kwao, hata uchafu ulikuwa mlo wenye ladha); wengine walikuwa wamejificha

misituni, lakini hawakusita kupumzika, kwani majimaji ndani ya majani yale ya kijani kizito ya kumetameta yaliwapa mlo wenye utomvu mwingi.... Baada ya wao kushiba, bado wadudu hawakusita kufanya shughuli zao; ingawa walikuwa wadogo kwa kimo, walimilikiwa na nishati ya ajabu pamoja na uchangamfu usio na mipaka, na kwa viumbe vyote wao ndio walikuwa amilifu zaidi na wenye bidii zaidi. Hawakuwahi kuwa wazembe, na hawakuhusika katika mapumziko yoyote. Baada ya kushiba, bado walifanya kazi na wakafanyiza miili yao bidii kwa minajili ya siku zao za usoni, wakiwa wamejishughulisha na kukimbia hapa na pale kwa minajili ya kesho yao ili waweze kuishi.... Kwa utaratibu waliweza kuimba nyimbo zenye midundo tofauti ili kuhimizana na kusihi kila mmoja wao aendelee na kazi. Waliweza pia kuongeza furaha kwenye nyasi, miti, na kila inchi ya udongo, huku wakifanya kila siku, na kila mwaka kuwa wa kipekee.... Wakiwa na lugha zao binafsi na kwa njia zao wenyewe, walipitisha taarifa kwa viumbe vyote vilivyokuwa ardhini. Na wakitumia mkondo wao binafsi maalum wa maisha, waliweka alama katika viumbe vyote, na baadaye wakaacha alama.... Walikuwa na uhusiano wa karibu sana na mchanga, nyasi, na misitu, na walipatia mchanga nguvu na uthabiti, vivyo hivyo kwenye nyasi, na misitu na wakaweza kuleta ushawishi na salamu za Muumba kwa viumbe hai vyote ...

Mtazamo wa Muumba ulienea kote kote kwenye viumbe vyote ambavyo Alikuwa ameumba na wakati huu kwa muda huo macho Yake yalitulizia misitu na milima, akili Yake ikigeuka. Huku matamshi Yake yakitamkwa wazi kwenye misitu mingi, na juu ya milima, kulionekana aina ya viumbe fulani vilivyokuwa tofauti na vyovyote vile vilivyokuwa vimekuja hapo awali: Walikuwa wanyama wa mwitu waliotamkwa kwa kinywa cha Mungu. Walikuwa wamepitiliza muda mrefu ajabu, walitikisa vichwa vyao na kupigapiga mikia yao, huku kila mmoja wao akiwa na uso wake pekee. Baadhi yao walikuwa na manyoya mengi, baadhi yao walikuwa wamejikinga, baadhi yao walikuwa na meno ya sumu, baadhi yao walikuwa wanakenua, baadhi yao walikuwa na shingo ndefu, baadhi yao walikuwa na mkia—mfupi, baadhi walikuwa na macho—mapana, baadhi walikuwa na mtazamo wa woga, baadhi walikuwa wamejiinamia ili wale nyasi, baadhi walikuwa na damu midomoni mwao, baadhi walikuwa wakidundadunda kwa miguu miwili, baadhi walikuwa wakirukaruka kwa kwato nne, baadhi walikuwa wakiangalia mbele juu ya mti, baadhi walikuwa wamejilalia tu wakisubiria misituni, baadhi walikuwa wakitafuta vyumba vya chini kwa chini ili kupumzika, baadhi walikuwa wakikimbiakimbia na kuonyesha furaha ya kipekee kwenye nchi tambarare, baadhi walikuwa wakinyatanyatia kwenye misitu...; baadhi walikuwa wakinguruma, baadhi walikuwa wakitoa milio mikali, baadhi walikuwa wakibweka, baadhi walikuwa wakilia...; baadhi walikuwa na sauti nyororo, baadhi walikuwa na sauti ya kati, baadhi walikuwa na sauti nzito, baadhi walikuwa na sauti safi na yenye mdundo wa kimuziki...; baadhi walikuwa wa kuogofya, na baadhi walikuwa warembo, na

baadhi walikuwa wakitisha, baadhi walikuwa wa kuvutia, baadhi walikuwa wa kutishia, baadhi walikuwa wasio na hatia ila wachangamfu.... Mmoja baada ya mwingine, wote walikuja. Tazama namna walivyotembea, kwenye uhuru, wasijue chochote kuhusu wenzao waliokuwa kando yao, wasitake hata kuchukua muda kutazamana.... Kila mmoja akiwa na maisha fulani waliyopewa na Muumba, na ukali wao binafsi, na ukatili, walionekana kwenye misitu na pia juu ya milima. Viumbe vya kudharauliwa kati ya vyote, na vyenye kuamrisha kabisa—ni nani aliyewafanya kuwa mabingwa wa kweli wa milimani na misituni? Kutoka muda ambao Kuonekana kwao kuliamriwa na Muumba, waliweza “kuweka madai” hayo katika misitu, na “kuweka madai” kwenye milima, kwani Muumba alikuwa tayari amepangilia mipaka yao na Akaamua upana wa uwepo wao. Hawa ndio waliokuwa mabwana wa kweli wa milimani na misitu, na ndiyo maana walikuwa na ukali mwingi na kwa hivyo wenye dharau. Waliitwa “wanyama wa mweituni” kimsingi kwa sababu, kati ya viumbe vyote, ndio waliokuwa wasiowezekana, wenye unyama, na wasiofugwa. Wasingeweza kufugwa, hivyo basi wasingeweza kulelewa na wasingeshi kwa amani na mapatano na mwanadamu au kufanya kazi kwa niaba ya mwanadamu. Ni kwa Sababu hawakuweza kufugwa, hawakuweza kumfanyia kazi mwanadamu, ndiyo maana iliwalazimu kuishi kwa umbali fulani kutoka kwa mwanadamu, na wasingeweza kusongelewa na mwanadamu. Kwa sababu hiyo, ilikuwa kwa sababu waliishi umbali fulani kutoka kwa mwanadamu, na wasingeweza kukaribiwa na mwanadamu ndiposa waliweza kutimiza wajibu wao waliopewa na Muumba: kuilinda milima na misitu. Ule ukali wao uliilinda milima na kulinda misitu, na ndio waliokuwa ulinzi bora zaidi na wenye hakikisho la uwepo wao na utekelezaji wao. Wakati uo huo, ukali wao uliendeleza na kuhakikisha usawazisho miongoni mwa viumbe vyote. Kuwasili kwao kulileta msaada na ukitaji mizizi kwenye milima na misitu; kuingia kwao kuliweza kuingiza nguvu na uthabiti zaidi kwenye milima ile mitupu na misitu mitupu. Kuanzia hapa kwenda mbele, milima na misitu ikawa ni makao yao ya kudumu, na wasingewahi kupoteza maskani yao, kwa sababu milima na misitu ilionekana na ikawepo kwa ajili yao, na wanyama wa mweituni wangetimiza wajibu wao na kufanya kila kitu ambacho wangeweza ili kuilinda. Kwa hivyo, pia, wanyama wa mweituni wangeweza kutii kwa umakinifu kule kusihwa na Muumba ili waweze kushikilia eneo lao, na kuendelea kutumia asili yao ya kinyama ili kuendeleza usawazisho wa viumbe vyote vilivyoanzishwa na Muumba, na kuonyesha waziwazi mamlaka na nguvu za Muumba!

Katika Mamlaka ya Muumba, Viumbe Vyote ni Timilifu

Viumbe vyote vilivyoubwa na Mungu, vikiwemo vile vilivyoweza kusonga na vile visingeweza kusonga, kama vile ndege na samaki, kama vile miti na maua, na hata ikiwemo mifugo, wadudu na wanyama wa mweituni, wote walioubwa kwenye siku ya sita—wote walikuwa wazuri mbele ya Mungu, na, vilevile, machoni mwa Mungu, viumbe hivi, kulingana

na mpango Wake, vilikuwa vimetimiza kilele cha utimilifu, navyo vilikuwa vimefikia viwango ambavyo Mungu alitaka kutimiza. Hatua kwa hatua, Muumba alifanya kazi Aliyoniua kufanya kulingana na mpango Wake. Kimoja baada ya kingine, vitu hivi Alivyonuia kuumba vilijitokeza, na kujitokeza kwa kila kiumbe kulikuwa onyesho la Mamlaka ya Muumba, na uthibitishaji wa mamlaka Yake, na kwa sababu ya uthibitishaji huu, viumbe vyote visingeweza kufanya chochote kingine ila kushukuru kwa neema ya Muumba na riziki ya Muumba. Huku vitendo hivi vya kimiujiza vya Mungu vikijionyesha, ulimwengu huu ulijaa, vipande kwa vipande, ukiwa na viumbe vyote vilivyoubwa na Mungu, na ukabadilika kutoka kwa fujo na giza hadi kwa wazi na uangavu, kutoka kwenye utulivu wa kutisha hadi kwa uchangamfu na nguvu zisizokuwa na mipaka. Miongoni mwa viumbe vyote vya uumbaji, kutoka kwa wale wakubwa hata wadogo, toka kwa wadogo hata kwa wale wadogo zaidi, hakuna hata kiumbe kimoja ambacho hakikuumbwa kupitia kwa Mamlaka na nguvu za Muumba, na kukawa na upekee na haja ya ndani kwa ndani na thamani ya uwepo wa kila kiumbe. Licha ya tofauti zao katika maumbo na muundo, lazima viumbe hivi vingeumbwa na Muumba ili viwepo chini ya mamlaka ya Muumba. Wakati mwingine watu wataona mdudu, yule aliye na sura mbaya kabisa na watasema, “Mdudu yule ni sura mbaya kweli, hakuna vile ambavyo kiumbe chenye sura mbaya kama hicho kinaweza kuwa kiliumbwa na Mungu—hakuna njia ambayo Angeumba kitu chenye sura mbaya hivyo.” Mtazamo wa kijinga kweli! Kile wanachofaa kusema ni, “Ingawa mdudu huyu ana sura mbaya sana, aliumbwa na Mungu, na kwa hivyo, lazima awe na kusudio lake la kipekee.” Kwenye fikira za Mungu, Aliniuia kupatia kila mojawapo ya sura, na kazi na matumizi aina zote, katika viumbe mbalimbali vilivyo na uhai Alivyoumba, na hivyo basi hamna kati ya viumbe hivyo ambavyo Mungu aliumba vilivyoubwa vikiwa vimefanana. Kuanzia sura yao ya nje hadi mkusanyiko wao wa ndani, kuanzia katika mazoea yao ya kuishi hadi mahali pa kuishi—kila kiumbe ni tofauti. Ng’ombe wana sura ya ng’ombe, punda wana sura ya punda, paa ana sura ya paa, na ndovu wana sura ya ndovu. Je, unaweza kusema ni kiumbe kipi kinachovutia zaidi na ni kipi kinachotisha zaidi kwa sura? Je, unaweza kusema ni kiumbe kipi chenye manufaa zaidi na uwepo wa kile ambacho hakihitajiki sana? Baadhi ya watu wanapenda namna ambavyo ndovu hufanana, lakini hakuna anayetumia ndovu kutayarisha mashamba ya kupanda: baadhi ya watu wanapenda namna simba na chui mkubwa mwenye milia walivyo, kwani sura inavutia zaidi miongoni mwa viumbe vyote, lakini je, unaweza kuwafuga nyumbani? Kwa ufupi, kuhusiana na viumbe vyote, binadamu anafaa kurejelea mamlaka ya Muumba, hivi ni kusema kwamba, rejelea mpangilio uliochaguliwa na Muumba katika viumbe vyote; huu ndio mtazamo wenye hekima zaidi. Mtazamo tu wa kutafuta, na wa kuwa mtiifu, kwa nia ama makusudio ya mwanzo ya Muumba ndio ukubalifu wa kweli na hakika wa mamlaka ya Muumba. Ni vyema kwa Muumba, kwa hivyo ni sababu gani ambayo binadamu atakuwa nayo ya kusema kwamba si vyema?

Hivyo basi, viumbe vyote vilivyo katika mamlaka ya Muumba vitaweza kucheza mdundo mpya wa ukuu wa Muumba, vitaanza utangulizi mwema kwa minajili ya kazi Yake kwenye siku mpya, na kwa muda huu Muumba ataufungua ukurasa mpya katika kazi ya usimamizi Wake! Kulingana na sheria ya mimea ya machipuko, kukomaa kwa kiangazi, mavuno ya mapukutiko, na hifadhi ya kipupwe iliyochaguliwa na Muumba, viumbe hivi vyote vitaweza kutilia mkazo mpango wa usimamizi wa Muumba na vitakaribisha siku yao mpya, mwanzo mpya, na mkondo mpya wa maisha, na hivi karibuni vitu vitaweza kuzaana katika mfululizo usioisha ili kuweza kukaribisha kila siku katika ukuu wa mamlaka ya Muumba ...

Hakuna Kiumbe Chochote Kati ya Vile Vilivyoumbwa na Vile Ambavyo Havikuumbwa Kinaweza Kubadilisha Utambulisho wa Muumba

Tangu Alipoanza uumbaji wa viumbe vyote, nguvu za Mungu zilianza kuonyeshwa na zikaanza kufichuliwa, kwani Mungu alitumia maneno kuumba vitu vyote. Haijalishi ni njia gani Alitumia, haijalishi ni kwa nini Aliviumba, viumbe vyote viliumbwa na kusimama imara na kuwepo kwa sababu ya matamshi ya Mungu, na haya ndiyo mamlaka ya kipekee ya Muumba. Kwenye muda kabla ya mwanadamu kuumbwa ulimwenguni, Muumba alitumia nguvu na mamlaka Yake kuumba viumbe vyote kwa minajili ya mwanadamu, na Akatumia mbinu za kipekee kutayarisha mazingira yanayofaa kuishi mwanadamu. Kwa yote Aliyoyafanya, ilikuwa ni kwa kumtayarishia mwanadamu ambaye hivi karibuni angepokea pumzi Zake. Hivi ni kusema kwamba, kwenye muda ule kabla ya mwanadamu kuumbwa, mamlaka ya Mungu yalionyesha kupitia kwenye viumbe vyote tofauti na mwanadamu, na vitu vikubwa kama vile mbingu, nuru, bahari, na ardhi, na vile vilivyo vidogo kama vile wanyama na ndege, pamoja na wadudu na vijiumbe vyote vya kila aina, zikiwemo vimelea mbalimbali visivyoonekana kwa macho ya kawaida. Kila mojawapo kilipewa maisha kwa matamshi ya Muumba, na kila kiumbe mojawapo kilizaana kwa sababu ya matamshi ya Muumba na kila kimojawapo kiliishi chini ya ukuu wa Muumba kwa sababu ya matamshi ya Muumba. Ingawa hawakupokea pumzi za Muumba, bado walionyesha maisha na nguvu walizopewa na Muumba kupitia kwa mifumo na miundo yao mbalimbali; Ingawa hawakupokea uwezo wa kuongea aliopewa mwanadamu na Muumba, kila kimojawapo kilipokea njia ya kuelezea maisha yao ambayo walipewa na Muumba, na ambayo ilitofautiana na ile lugha ya Mwanadamu. Mamlaka ya Muumba hayatoi tu nguvu za maisha kwenye vifaa vinavyoonekana kuwa tuli, ili visiwahi kutoweka, lakini, vilevile, hupatia silika ya kuzaana na kuongezeka kwa kila kiumbe hai, ili visiwahi kutoweka, na ili kizazi baada ya kizazi, vitaweza kupitisha sheria na kanuni za kuishi walizopewa na Muumba. Namna ambavyo Muumba anatilia mkazo mamlaka Yake haikubaliani kwa lazima na mtazamo wa mambo makubwa makubwa au madogomadogo, na haiwekewi mipaka ya umbo lolote; Anaweza kuamuru utendaji mambo katika ulimwengu na kushikilia ukuu juu ya maisha na kifo cha

viumbe vyote, na, vilevile, Anaweza kushughulikia viumbe vyote ili viweze kumhudumia Yeye; Anaweza kusimamia kazi zote za milima, mito, na maziwa, na kutawala viumbe vyote ndani yake, na, zaidi ya hayo, Anaweza kutoa kile ambacho kinahitajika na viumbe vyote. Haya ndiyo maonyesho ya mamlaka ya pekee ya Muumba miongoni mwa viumbe vyote mbali na mwanadamu. Maonyesho kama hayo si tu ya maisha tunayoishi, na hayatawahi kusita, au kupumzika, na hayawezi kubadilishwa au kuharibiwa na mtu yeyote au kitu chochote, wala hayawezi kuongezwa au kupunguzwa na mtu yeyote au kitu chochote—kwani hamna kile kinachoweza kubadilisha utambulisho wa Muumba, na, hivyo basi, mamlaka ya Muumba hayawezi kubadilishwa na kiumbe chochote kilichoumbwa, na hayawezi kufikiwa na kiumbe chochote ambacho hakikuumbwa. Chukulia wajumbe na malaika wa Mungu kwa mfano. Hawamiliki nguvu za Mungu, isitoshe hawamiliki mamlaka ya Muumba, na sababu ambayo hawana nguvu na mamlaka ya Mungu ni kwa sababu hawamiliki ile hali halisi ya Muumba. Vile viumbe ambavyo havikuumbwa, kama vile wajumbe na malaika wa Mungu, Ingawa vinaweza kufanya baadhi ya mambo kwa niaba ya Mungu, haviwezi kuwakilisha Mungu. Ingawa wanamiliki nguvu fulani zisizomilikiwa na binadamu, hawamiliki mamlaka ya Mungu, hawamiliki mamlaka ya Mungu ya kuumba viumbe vyote, na kuamuru viumbe vyote, na kushikilia kuwa na ukuu juu ya viumbe vyote. Na kwa hivyo upekee wa Mungu hauwezi kubadilishwa na kiumbe chochote ambacho hakikuumbwa, na vilevile, mamlaka na nguvu za Mungu haviwezi kusawazishwa na kiumbe chochote ambacho hakikuumbwa. Kwenye Biblia, je, umewahi kusoma kuhusu mjumbe yeyote wa Mungu aliyeumba viumbe vyote? Na kwa nini Mungu hakuwahi kutuma mmojawapo wa wajumbe Wake au malaika kuumba viumbe vyote? Kwa sababu hawakumiliki mamlaka ya Mungu, na kwa hivyo hawakumiliki uwezo wa kutekeleza mamlaka ya Mungu. Sawa tu na viumbe vyote, viumbe vyote visivyoubwa viko chini ya ukuu wa Muumba, na chini ya mamlaka ya Muumba, na kwa hivyo, kwa njia ile ile, Muumba pia ni Mungu wao na pia ndiye Mtawala wao. Miongoni mwa kila mmoja wao—haijalishi kama wao ni sharifu au kina yahe, wenye nguvu nyingi au kidogo—hakuna hata mmoja anayeweza kuzidi mamlaka ya Muumba, na kwa hivyo miongoni mwao, hakuna hata mmoja wao anayeweza kubadilisha utambulisho wa Muumba. Hawatawahi kuitwa Mungu, na hawatawahi kuweza kuwa Muumba. Huu ni ukweli na hoja zisizobadilika!

Kupitia ushirika uliotajwa hapo juu, je, tunaweza kusema yafuatayo: Muumba na Kiongozi wa viumbe vyote tu, Yule anayemiliki mamlaka ya kipekee na nguvu za kipekee, ndiye Anayeweza kuitwa Mungu Mwenyewe wa kipekee? Wakati huu, unaweza kuhisi kwamba swali kama hilo ni la kina sana. Wewe, kwa muda huu, huwezi kulielewa, na huwezi kung'amua kiini cha ndani na kwa hivyo kwa muda huu unahisi kwamba ni swali gumu kujibu. Kwa hivyo, Nitaendelea na ushirika Wangu. Kinachofuata, Nitakuruhusu kutazama vitendo halisi vya dhana

nyingi za mamlaka na nguvu zinazomilikiwa na Mungu pekee, na hivyo basi Nitakuruhusu kuelewa kwa kweli, kushukuru, na kujua upekee wa Mungu, na maana ya mamlaka ya kipekee ya Mungu.

2. Mungu Hutumia Matamshi Yake Kuanzisha Agano na Binadamu

Mwa 9:11-13 Na nitaweka agano langu na ninyi, wala miili yote haitaondolewa tena na maji ya gharika; wala hakutakuwa na gharika tena kuiharibu dunia. Naye Mungu akasema, Hii ni alama ya agano ambayo naifanya kati ya Mimi na ninyi na viumbe vyote vyenye uhai vilivyo nanyi, kwa vizazi vya kudumu: naweka upinde wangu mawinguni, na utakuwa alama ya agano kati ya Mimi na dunia.

Baada ya Kuumba Viumbe Vyote, Mamlaka ya Muumba Yanathibitishwa na Kuonyeshwa kwa Mara Nyingine Tena Kwenye Agano la Upinde wa Mvua

Mamlaka ya Muumba siku zote yanaonyeshwa na kutekelezwa miongoni mwa viumbe vyote, Naye hatawali tu hatima ya viumbe vyote, lakini pia Anatawala mwanadamu, kiumbe maalum ambacho Aliumba kwa mikono Yake mwenyewe, na kinachomiliki muundo tofauti wa uhai na kinachopatikana kwa mfumo tofauti wa uhai. Baada ya kuumba viumbe vyote, Muumba hakusita kuonyesha mamlaka na nguvu Zake; kwake Yeye, mamlaka ambayo Alishikilia ukuu juu ya viumbe vyote na hatima ya mwanadamu kwa ujumla, ilianza rasmi tu pale ambapo mwanadamu alizaliwa kwa kweli kutoka kwenye mkono Wake. Alinuia kusimamia mwanadamu, kutawala mwanadamu, Alinuia kumwokoza mwanadamu, Alinuia kufaidi mwanadamu kwa kweli, kufaidi mwanadamu ambaye angetawala viumbe vyote, na Alinuia kumfanya mwanadamu kama huyo kuishi chini ya mamlaka Yake, na kujua mamlaka Yake, na kutii mamlaka Yake. Hivyo basi, Mungu akaanza kuonyesha rasmi mamlaka Yake miongoni mwa binadamu kwa kutumia matamshi Yake, na Akaanza kutumia mamlaka Yake kutambua matamshi Yake. Bila shaka, mamlaka ya Mungu yalionyeshwa mbele katika sehemu zote wakati wa mchakato huu; Nimeweza kuchukua tu baadhi ya mifano mahususi, inayojulikana ambayo unaweza kuelewa na kujua upekee wa Mungu na kuelewa na kujua upekee wa mamlaka ya Mungu.

Kunao mfanano kati ya fungu kwenye Mwanzo 9:11-13 na Mafungu yaliyo hapo juu yanayohusu rekodi za Mungu kuumba ulimwengu, ilhali kunayo pia tofauti. Mfanano ni upi? Mfanano umo katika matumizi ya matamshi na Mungu kuweza kufanya kile ambacho Alinuia, na tofauti ni kwamba, fungu hili ni mazungumzo ya Mungu na binadamu, ambapo Alianzisha agano na binadamu, na Akamwambia binadamu kuhusu kile ambacho kilikuwa ndani ya agano hilo. Utiliaji mkazo huu wa mamlaka ya Mungu ulitimizwa wakati wa mazungumzo Yake na

Mungu, hivi ni kusema kwamba, kabla ya uumbaji wa mwanadamu, maneno ya Mungu yalikuwa maagizo, na amri ambavyo vilitolewa kwa viumbe ambavyo Alinua kuumba. Lakini sasa kulikuwa na mtu wa kusikiliza matamshi ya Mungu, na hivyo basi matamshi Yake yalikuwa ya mazungumzo na binadamu, na pia himizo na onyo kwa binadamu, na zaidi, kulikuwa na amri zilizotolewa kwa viumbe vyote vilivyokuwa na mamlaka Yake.

Ni hatua gani ya Mungu imerekodiwa katika fungu hili? Inarekodi agano ambalo Mungu alianzisha na binadamu baada ya Yeye kuangamiza ulimwengu kwa gharika, linamwambia binadamu kwamba Mungu asingesababisha maangamizo katika ulimwengu tena, na kwamba, hadi mwisho huu, Mungu aliumba ishara—na ishara hii ilikuwa nini? Kwenye Maandiko inasemekana kwamba “naweka upinde wangu mawinguni, na utakuwa alama ya agano kati ya Mimi na dunia.” Haya ni matamshi ya asili yaliyotamkwa na Muumba kwa mwanadamu. Aliposema matamshi haya, upinde wa mvua ulionekana mbele ya macho ya binadamu, ambapo ulibakia mpaka leo. Kila mmoja ameuona upinde wa mvua kama huo, na unapouona, je, unajua namna unavyojitokeza? Sayansi haiwezi kuthibitisha haya, au kutafuta chanzo chake, au kutambua mambo yanayosababisha upinde huu wa mvua. Hiyo ni kwa sababu, upinde wa mvua ni ishara ya agano lilioanzishwa kati ya Muumba na binadamu; hauhitaji msingi wowote wa kisayansi, haukuumbwa na binadamu, wala binadamu hawezi kuubadilisha. Ni maendelezo ya mamlaka ya Muumba baada ya Yeye kuongea matamshi Yake. Muumba alitumia mbinu fulani Yake mwenyewe kutii agano lake na binadamu na ahadi Yake, na hivyo basi matumizi Yake ya upinde wa mvua kama ishara ya agano ambalo Alianzisha ni maelekezo na sheria ya mbinguni yatakayobakia milele hivyo, haijalishi kama ni kuhusiana na Muumba au mwanadamu aliyeumbwa. Ilhali sheria hii isiyobadilika ni, lazima isemwe, maonyesho mengine ya kweli ya mamlaka ya Muumba kufuatia uumbaji Wake wa viumbe vyote, na lazima isemwe kwamba mamlaka na nguvu za Muumba havina mipaka; matumizi Yake ya upinde wa mvua ni ishara ya maendelezo na upanuzi wa mamlaka ya Muumba. Hiki kilikuwa kitendo kingine kilichotekelezwa na Mungu kwa kutumia matamshi Yake, na kilikuwa ni ishara ya agano ambalo Mungu alikuwa ameanzisha na mwanadamu kwa kutumia matamshi. Alimwambia binadamu kuhusu kile ambacho Aliamua kuleta, na kwa njia gani kingekamilishwa na kutimizwa, na kwa njia hii suala liliweza kutimizwa kulingana na matamshi kutoka kwenye kinywa cha Mungu. Mungu pekee ndiye anayemiliki nguvu kama hizo, na leo, miaka elfu kadhaa baada ya Yeye kuongea matamshi haya, binadamu angali bado anaweza kuangalia upinde wa mvua uliozungumziwa kutoka kwenye kinywa cha Mungu. Kwa sababu ya matamshi hayo yaliyotamkwa na Mungu, kitu hiki kimebakia bila ya kusongezwa na kubadilishwa mpaka hadi leo. Hakuna anayeweza kuuondoa upinde huu wa mvua, hakuna anayeweza kubadilisha sheria zake, na upo kimsingi kutokana na matamshi ya Mungu. Haya kwa hakika ni mamlaka ya

Mungu. “Mungu ni mzuri tu kama matamshi Yake, na matamshi Yake yataweza kukamilishwa, na kile ambacho kimekamilishwa kinadumu milele.” Matamshi kama haya kwa kweli yanaonyeshwa waziwazi hapa, na ni ishara na sifa wazi kuhusu mamlaka na nguvu za Mungu. Ishara au sifa kama hiyo haimilikiwi na au kuonekana katika viumbe vyovyote vile vilivyoumbwa, wala kuonekana kwenye viumbe vyovyote vile ambavyo havikuumbwa. Inamilikiwa tu na Mungu wa kipekee, na inapambanua utambulisho na hali halisi inayomilikiwa tu na Muumba kutoka ile ya viumbe. Wakati uo huo, ni ishara na sifa pia ambayo mbali na Mungu Mwenyewe, haitawahi kupitwa na kiumbe chochote kilichoumbwa au kile ambacho hakikuumbwa.

Uanzishaji wa agano Lake Mungu na binadamu kilikuwa ni kitendo chenye umuhimu mkubwa, na ambao Alinuia kutumia ili kuwasilisha hoja kwa binadamu na kumwambia binadamu mapenzi Yake, na hadi hapa, Alitumia mbinu ya kipekee, kwa kutumia ishara maalum ya kuanzisha agano na binadamu, ishara ambayo ilikuwa ahadi ya agano ambalo Alikuwa ameanzisha na binadamu. Kwa hivyo, je, uanzishaji wa agano hili ulikuwa ni tukio kubwa? Na tukio hili lilikuwa kubwa vipi? Hii haswa ndiyo inayoonyesha namna ambavyo agano hili lilivyo maalum: si agano lililoanzishwa kati ya binadamu mmoja na mwingine, au kundi moja na jingine, au nchi moja na nyingine, lakini agano lililoanzishwa kati ya Muumba na wanadamu kwa ujumla, na litabakia halali mpaka siku ambayo Muumba atakomesha mambo yote. Mtekelezaji wa agano hili ni Muumba, na mwendelezaji pia ni Muumba. Kwa ufupi, uzima wa agano la upinde wa mvua ulioanzishwa pamoja na mwanadamu ulikamilishwa na kutimizwa kulingana na mazungumzo kati ya Muumba na mwanadamu, na umebakia vivyo hivyo mpaka leo. Ni nini kingine ambacho viumbe vinaweza kufanya mbali na kujinyenyekeza, na kutii, na kusadiki, na kushukuru, na kutolea ushuhuda, na kusifu mamlaka ya Muumba? Kwani hamna yeyote yule isipokuwa Mungu wa pekee anayemiliki nguvu za kuanzisha agano kama hilo. Kujitokeza kwa upinde wa mvua mara kwa mara, kunatangaza kwa mwanadamu na kumtaka azingatie agano lile kati ya Muumba na mwanadamu. Katika kujitokeza kwingine kwa agano kati ya Muumba na binadamu, kile kinachoonyeshwa kwa mwanadamu si upinde wa mvua au agano lenyewe, lakini ni mamlaka yenyewe yasiyobadilika ya Muumba. Kujitokeza kwa upinde wa mvua, mara kwa mara, kunaonyesha yale matendo ya kipekee na ya kimiujiza ya Muumba yanayopatikana kwenye sehemu zilizofichwa, na, wakati uo huo ni onyesho muhimu la mamlaka ya Muumba ambayo hayatawahi kufifia, na wala kubadilika. Je, hili si onyesho la dhana nyingine ya mamlaka ya kipekee ya Muumba?

3. Baraka za Mungu

Mwa 17:4-6 Na kuhusu mimi, tazama, agano langu liko na wewe, na wewe utakuwa baba

yao mataifa mengi. Nalo jina lako halitakuwa Abramumu tena, ila jina lako litaitwa Ibrahimu; kwa kuwa nimekufanya uwe baba yao mataifa mengi. Na Mimi nitafanya uwe na uzao ulio mwingi mno, na nitayaunda mataifa kutoka kwako, nao wafalme watatoka kwako.

Mwa 18:18-19 Ibrahimu hakika atakuwa taifa kubwa na lenye nguvu, na mataifa yote ya dunia yatabarikiwa kupitia yeye. Kwani namjua, kuwa atawatawala watoto wake na nyumba yake kufuata yeye, na wataishika njia ya Yehova, kufanya haki na hukumu; ili Yehova aweze kumletea Ibrahimu yale ambayo amemwambia.

Mwa 22:16-18 Mimi nimeapa kujipitia, akasema Yehova, kwa maana umefanya jambo hili, na hujamzuilia mwana wako, mwana wako wa pekee: Kuwa katika kubariki nitakupa baraka, na katika kuzidisha uzao wako nitazidisha mithili ya nyota za mbinguni, na mithili ya mchanga uliopo kwenye ukanda wa pwani; na uzao wako utakuwa na mlango wa maadui zao; Na kupitia uzao wako kila taifa la dunia litabarikiwa; kwa kuwa umeitumikia sauti yangu.

Ayu 42:12 Kwa hivyo Yehova akabariki mwisho wa baadaye wa Ayubu zaidi kuliko mwanzo wake: kwa sababu alikuwa na kondoo elfu kumi na nne, na ngamia elfu sita, na elfu moja ya jozi za ng'ombe, na elfu moja ya punda wa kike.

Njia na Sifa za Kipekee za Matamshi ya Muumba Ni Ishara ya Utambulisho na Mamlaka ya Kipekee ya Muumba

Wengi hupenda kutafuta, na kufaidi, baraka za Mungu, lakini si kila mmoja anayeweza kufaidi baraka hizi, kwani Mungu anazo kanuni Zake binafsi, na Yeye hubariki binadamu kulingana na njia Zake binafsi. Ahadi ambazo Mungu hutoa kwa binadamu, na kiwango cha neema ambacho Yeye humpa binadamu, vyote vinatolewa kulingana na fikira na vitendo vya binadamu. Hivyo, ni nini huonyeshwa kupitia kwa baraka za Mungu? Watu wanaweza kuona nini ndani yake? Wakati huu, hebu tuweke kando mazungumzo kuhusu ni aina gani ya watu ambao Mungu hubariki, na kanuni anazofuata Mungu katika kubariki binadamu. Badala yake, hebu tuangalie baraka za Mungu kwa binadamu kwa kusudio la kujua mamlaka ya Mungu, kutoka kwenye mtazamo wa kujua mamlaka ya Mungu.

Mafungu manne ya maandiko yaliyotajwa hapo juu yote ni rekodi kuhusu baraka za Mungu kwa binadamu. Yanatupa ufafanuzi wenye maelezo kuhusu wapokeaji wa baraka za Mungu, kama vile Ibrahimu na Ayubu, vilevile yanatupa sababu zinazoelezea kwa nini Mungu alitoa baraka Zake, na ni nini kilichokuwa kwenye baraka hizi. Ile sauti na njia ya matamshi ya Mungu, mtazamo na mahali ambapo Alitamka, huturuhusu kushukuru kwamba Yule anayetoa baraka na mpokeaji wa baraka kama hizo ni wenye utambulisho, hadhi, na hali halisi tofauti kabisa. Sauti na njia ambayo matamshi haya yanatolewa, na mahali ambapo yalitamkwa, vinaonyesha upekee

wao kwa Mungu, anayemiliki utambulisho wa Muumba. Anayo mamlaka na uwezo, pamoja na heshima ya Muumba, na adhama isiyovumilia shaka kutoka kwa binadamu yeyote.

Kwanza hebu tuangalie Mwa 17:4-6: “Na kuhusu mimi, tazama, agano langu liko na wewe, na wewe utakuwa baba yao mataifa mengi. Nalo jina lako halitakuwa Abram tena, ila jina lako litaitwa Ibrahimu; kwa kuwa nimekufanya uwe baba yao mataifa mengi. Na Mimi nitafanya uwe na uzao ulio mwingi mno, na nitayaunda mataifa kutoka kwako, nao wafalme watatoka kwa wewe.” Matamshi haya ndiyo yaliyokuwa agano ambalo Mungu alianzisha na Ibrahimu, pamoja na baraka za Mungu kwa Ibrahimu: Mungu angemfanya Ibrahimu baba wa mataifa, Angemfanya kuwa na uzao mwingi, na Angemfanya kuwa na mataifa mengi, nao wafalme wangetoka kwake. Je, unayaona mamlaka ya Mungu katika maneno haya? Na unayaonaje mamlaka kama hayo? Ni dhana gani ya hali halisi ya mamlaka ya Mungu unayoona? Kutoka kwa usomaji wa makini wa maneno haya, si vigumu kutambua kwamba mamlaka na utambulisho wa Mungu vyote vimefichuliwa waziwazi na maneno ya matamshi ya Mungu. Kwa mfano, Mungu anaposema “agano langu liko na wewe, na wewe utakuwa ... kuwa nimekufanya ... Mimi nitafanya uwe...,” kauli kama vile “wewe utakuwa” na “nitayaunda,” ambazo maneno yake yanasheheni thibitisho la utambulisho na mamlaka ya Mungu, kwa upande mmoja ni onyesho la uaminifu wa Muumba; kwa upande mwingine, ni maneno maalum yaliyotumiwa na Mungu, anayemiliki utambulisho wa Muumba—pamoja na kuwa sehemu ya msamiati uliozoeleka. Kama mtu atasema anatumai kuwa mtu mwingine atazidisha uzao, kwamba mataifa yatatokana na wao, na kuwa wafalme watatoka miongoni mwao, basi hiyo bila shaka ni aina ya tamania, na si ahadi wala baraka. Na hivyo, hawathubutu kusema “Mimi nitakufanya kuwa hivi na hivi, kutafanya hivi na hivi...,” kwani wanajua kwamba hawamiliki nguvu kama hizo; si juu yao, na hata kama watasema maneno kama hayo, maneno yao yatakuwa matupu, na ya kipuzi, yanayoendeshwa na matamania na maono yao. Je, yupo yeyote anayethubutu kungea kwa sauti kuu kama hiyo ilhali wanahisi kwamba hawawezi kutimiza matamania yao? Kila mtu hutamani mema yafikie kizazi chake, na kutumai kwamba kitafanikiwa na kufurahia ufanisi mkubwa. “Ni utajiri upi mkubwa utakaokuwepo kama mmoja wao angekuwa mfalme mkuu! Kama mmoja angekuwa gavana ingekuwa vizuri, pia—mradi tu wawe ni watu muhimu!” Haya yote ni matamania ya watu wote, lakini watu wanaweza kutamani tu baraka juu ya kizazi chao, na hawawezi kutimiza au kufanya ahadi zao zozote kuwa kweli. Katika mioyo yao, kila mtu anajua waziwazi kwamba wao hawamiliki nguvu za kutimiza mambo kama hayo, kwani kila kitu chao ni zaidi ya udhibiti wao, na hivyo basi watawezaje kuamuru hatima ya wengine? Sababu inayomfanya Mungu kusema mambo kama haya ni kwa vile Mungu anamiliki mamlaka kama hayo, na Anaweza kutekeleza na kutambua ahadi zote Anazotoa kwa ajili ya binadamu, na kufanya baraka zote Anazomwomba binadamu kuwa kweli. Binadamu aliumbwa na Mungu, na ili Mungu aweze

kumuumba mtu atakayezidi kwa uzao ni jambo ambalo litakuwa rahisi sana; kufanya kizazi cha mtu kufanikiwa kutahitaji neno moja tu kutoka Kwake. Hatawahi kufanya kazi Mwenyewe na kutoa jasho kwa ajili ya kitu kama hicho, au kushughulisha akili Yake, au kujifunga mafunda mbalimbali; hii ndiyo nguvu halisi ya Mungu, mamlaka halisi ya Mungu.

Baada ya kusoma “Ibrahima hakika atakuwa taifa kubwa na lenye nguvu, na mataifa yote ya dunia yatabarikiwa kupitia yeye” kwenye Mwanzo 18:18, je, unaweza kuhisi mamlaka ya Mungu hapo? Unaweza kuhisi hali isiyokuwa ya kawaida ya Muumba? Unaweza kuhisi hali ya mamlaka ya juu ya Muumba? Maneno ya Mungu yana uhakika. Mungu hasemi maneno kama hayo kwa sababu ya, au kwa kuwakilisha, ujasiri Wake katika ufanisi; hayo ni, badala yake, ithibati ya mamlaka ya matamshi, na ni amri inayotimiza maneno ya Mungu. Kunazo semi mbili ambazo unafaa kutilia maanani hapa. Wakati Mungu anaposema “Ibrahima hakika atakuwa taifa kubwa na lenye nguvu, na mataifa yote ya dunia yatabarikiwa kupitia yeye,” kunayo dalili ya kutoeleweka kwenye maneno haya? Kunayo dalili yoyote ya wasiwasi? Kunayo dalili yoyote ya woga? Kwa sababu ya matamshi “ataweza kwa hakika” na “atakuwa” kwenye matamshi ya Mungu, dalili hizi, ambazo zinapatikana tu kwa binadamu na mara nyingi zinajionyesha ndani yake, hazijawahi kupata uhusiano wowote na Muumba. Hakuna mtu angethubutu kutumia maneno kama haya wakati akiwatakiwa wengine mema, hakuna yule angethubutu kubariki mwingine apate taifa kubwa na lenye nguvu kwa uhakika kama huo, au kutoa ahadi kwamba mataifa yote ya dunia yatabarikiwa kupitia kwake. Maneno ya Mungu yanapokuwa na uhakika zaidi, ndipo yanathibitisha kitu fulani—na kitu hicho ni nini? Yanathibitisha kuwa Mungu anayo mamlaka kama hayo, kuwa mamlaka Yake yanaweza kutimiza mambo haya, na kwamba ufanisi wake ni lazima. Mungu alikuwa na uhakika katika moyo Wake, bila kusita kokote, kwa kila kitu Alichombariki Ibrahimu. Aidha, uzima wa haya utakamilishwa kulingana na maneno Yake, na hakuna nguvu ingeweza kubadilisha, kuzuia, kuharibu, au kutatiza kukamilika kwake. Licha ya kilichotendeka, hakuna kitu ambacho kingebatilisha au kuathiri kutimia na kukamilika kwa matamshi ya Mungu. Huu ndio uzito wenyewe wa maneno yaliyotamkwa kutoka kinywa cha Muumba, na mamlaka ya Muumba ambayo hayavumilii kanusho la binadamu! Baada ya kuyasoma maneno haya, ungali unahisi shaka? Maneno haya yalitamkwa kutoka kinywa cha Mungu, na kunazo nguvu, adhama na mamlaka katika maneno ya Mungu. Uwezo na mamlaka kama haya, na kutozuilika kwa kukamilika kwa hoja, haviwezi kufikiwa na kiumbe chochote kilichoumbwa au kile ambacho hakikuumbwa na haviwezi kupitwa na kiumbe chochote kilichoumbwa au kile ambacho hakikuumbwa. Muumba pekee ndiye anaweza kuongea na binadamu kwa sauti na mkazo kama huo, na hoja zimethibitisha kuwa ahadi Zake si maneno matupu, au majigambo ya kupitisha wakati, lakini ni maonyesho ya mamlaka ya kipekee yasiyoweza kupitwa na mtu, kitu, au kifaa chochote.

Ni nini tofauti kati ya maneno yanayotamkwa na Mungu na yale yanayotamkwa na binadamu? Unaposoma maneno haya yaliyotamkwa na Mungu, unahisi nguvu za maneno ya Mungu, na mamlaka ya Mungu. Je, unahisi vipi unaposikia watu wakitamka maneno kama hayo? Je, unafikiria kuwa wao wana kiburi kupindukia, na ni wenye kujigamba na kujionyesha? Kwani hawana nguvu hizi, hawamiliki mamlaka kama haya, na hivyo basi hawawezi kabisa kutimiza mambo kama hayo. Kwamba wao wana hakika kabisa kuhusu ahadi zao, yaonyesha tu kutojali kwa matamshi yao. Kama mtu anasema maneno kama hayo, basi bila shaka watakuwa wenye kiburi, na waliozidisha ujasiri wao, huku wakijifichua kama mfano wa pekee wa tabia ya malaika mkuu. Maneno haya yalitoka kinywani mwa Mungu; je, unahisi dalili yoyote ya kiburi hapa? Je, unahisi ya kwamba matamshi ya Mungu ni mzaha tu? Matamshi ya Mungu ni mamlaka, Maneno ya Mungu ni hoja za kweli, na kabla hajatamka maneno kutoka kinywani Mwake, hivi ni kusema, wakati Anapofanya uamuzi wa kufanya kitu, tayari kitu hicho kimefanyika. Yaweza kusemwa kwamba kila kitu alichosema Mungu kwa Ibrahimu kilikuwa agano ambalo Mungu alianzisha na Ibrahimu, na ahadi Alizotoa kwa Ibrahimu. Ahadi hii ilikuwa hoja iliyoanzishwa, pamoja na hoja iliyokamilika, na hoja hizi zilitimizwa kwa utaratibu kwa fikira za Mungu kulingana na mpango wa Mungu. Kwa hivyo, Mungu kusema maneno kama hayo haimaanishi kuwa Ana tabia ya kiburi, kwani Mungu anaweza kutimiza mambo kama hayo. Anazo nguvu na mamlaka, na ana uwezo wa kutimiza hoja hizi, na mafanikio yake kwa jumla yanapatikana ndani ya uwezo Wake. Wakati maneno kama haya yanapotamkwa kutoka kwenye kinywa cha Mungu, yanakuwa ufunuo na maonyesho ya tabia ya kweli ya Mungu, ufunuo na maonyesho timilifu ya hali halisi na mamlaka ya Mungu, na hakuna kitu ambacho kinafaa zaidi na kizuri kama ithibati ya utambulisho wa Mungu. Namna, sauti, na mpangilio wa maneno ya matamshi kama hayo ndiyo alama haswa ya utambulisho wa Muumba, na vyote hivi vinalingana kwa njia timilifu na maonyesho na utambulisho wa Mungu, na ndani yao hakuna kusingizia, au kasoro; vyote hivi ni, onyesho timilifu na lililo kamili kabisa, la hali halisi na mamlaka ya Muumba. Lakini Kuhusu viumbe, havimiliki mamlaka haya, wala hali hii halisi, vilevile havimiliki nguvu inayotolewa na Mungu. Kama binadamu atasaliti tabia kama hiyo, basi hali hiyo itakuwa bila shaka mlipuko wa tabia yake iliyopotoka, na itaishia kwa athari ya kujihusisha visivyofaa na kiburi cha binadamu na maono yasiyo na mipaka, na kufichuliwa kwa nia haribifu za yuleyule ibilisi, Shetani, anayependa kudanganya watu na kuwashawishi kuweza kusaliti Mungu. Naye Mungu anachukuliaje kile ambacho kimefichuliwa kwa lugha kama hii? Mungu angesema kwamba ungependa kunyakua nafasi Yake na kwamba unapenda kumwiga Yeye na kumbadili Yeye. Wakati unaiga sauti ya matamshi ya Mungu, nia yako ni ya kubadilisha mahali pa Mungu katika mioyo ya watu, kujitwalia mwanadamu ambaye anamilikiwa kwa haki na Mungu. Huyu ni Shetani, wazi na bila kukuficha; haya ni matendo ya vizazi vya malaika mkuu visivyovumilika Mbinguni! Miongoni mwenu, kunao wowote waliowahi kuiga Mungu kwa njia fulani kwa

kuongea maneno machache, kwa nia ya kupotosha na kudanganya watu na kuwafanya watu kuhisi kuwa maneno na matendo ya mtu huyu yana mamlaka na nguvu za Mungu, kama kwamba hali halisi na utambulisho wa mtu huyo ni vya upekee, na hata ni kana kwamba sauti ya mtu huyu ni sawa na ile ya Mungu? Umewahi kufanya jambo kama hili? Umewahi kuiga sauti ya Mungu kwenye matamshi yako, kwa miondoko iliyodai kuwakilisha tabia za Mungu, ikiwa pamoja na uwezo na mamlaka ya kudhaniwa? Je, wengi wenu huwa mara nyingi mnatenda, au kupanga kutenda kwa njia kama hiyo? Sasa, unapooni kwa kweli, kuelewa na kujua mamlaka ya Muumba, na kutazama kile ulichokuwa ukikifanya, na ulichokuwa ukifichua kujihusu, je, unahisi vibaya? Je, unatambua hali yako ya kutoheshimu na kuwa na utovu wa haya? Baada ya kuchambua tabia na hali halisi ya watu kama hawa, je, inaweza kusemekana kuwa wao ndio walaaniwa wa jahanamu? Yaweza kusemekana kuwa kila mtu anayefanya mambo kama haya anajiletea udhalilishaji? Je, unatambua uzito wa asili yake? Na uzito wake ni wa kiasi kipi? Nia ya watu wanaotenda mambo kwa njia hii ni kuiga Mungu. Wanataka kuwa Mungu, na kuwafanya watu kuwaabudu kama Mungu. Wanataka kuondoa nafasi ya Mungu katika mioyo ya watu, na kutupilia mbali yule Mungu anayefanya kazi miongoni mwa binadamu, ili kutimiza nia ya kuwadhibiti watu, na kuwateketeza watu, na kuwamiliki watu hao. Kila mmoja anayo matamano na maono kama hayo yaliyofichika akilini, na kila mmoja anaishi katika hali halisi potovu na ya kishetani kama hiyo na anaishi katika asili ya kishetani ambapo yumo katika uadui na Mungu, na anamsaliti Mungu, na anapenda kuwa Mungu. Kufuatia Ushirika Wangu katika mada hii ya Mungu, bado ungependa au ungetamani kujifanya wewe ni Mungu, au kuiga Mungu? Na bado unatamani kuwa Mungu? Ungali unapenda kuwa Mungu? Mamlaka ya Mungu hayawezi kuigwa na binadamu, na utambulisho na hadhi ya Mungu haiwezi kuigizwa na binadamu. Ingawa unaweza kuiga sauti ambayo Mungu huongea nayo, huwezi kuiga hali halisi ya Mungu. Ingawa unaweza kusimama mahali pa Mungu na kujifanya kuwa Mungu, hutawahi kuweza kufanya kile ambacho Mungu ananua kukifanya, na hutawahi kutawala na kuamuru viumbe vyote. Katika macho ya Mungu, utabakia kuwa kiumbe kidogo, na haijalishi ni vipi ambavyo mbinu na uwezo wako ulivyo mkubwa, haijalishi ni vipaji vingapi unavyo, uzima wako wewe umetawaliwa na Muumba. Ingawa unaweza kusema maneno fulani ya kijeuri, hilo haliwezi kuonyesha kuwa unayo hali halisi ya Muumba, wala kuwakilisha ya kwamba unamiliki mamlaka ya Muumba. Mamlaka na nguvu za Mungu ni hali halisi ya Mungu Mwenyewe. Hayakufunzwa wala kusomwa, au kuongezewa kutoka nje, lakini ni hali ya asili ya Mungu Mwenyewe. Na kwa hivyo uhusiano kati ya Muumba na viumbe hauwezi katu kubadilishwa. Kama mojawapo ya viumbe, lazima mwanadamu achukue nafasi yake mwenyewe, na ajiendeleze kwa uangalifu, na kulinda kwa wajibu kile ambacho ameaminiwa na Muumba. Naye binadamu lazima asitende mambo nje ya mipaka yake au kufanya mambo zaidi ya uwezo wake au kufanya mambo ambayo ni ya kuchukiza Mungu. Binadamu ni lazima asijaribu kuwa

mkubwa, au wa kipekee, au zaidi ya wengine, wala asitafute kuwa Mungu. Hivi ndivyo watu hawafai kutamani kuwa. Kutamani kuwa mkubwa au wa kipekee ni jambo la upuuzi. Kutafuta kuwa Mungu ndilo hata jambo la aibu zaidi; linaudhi na linastahili kudharauliwa. Kile cha kupongezwa, na ambacho viumbe vinastahili kushikilia kuliko chochote kile ni kuwa viumbe vya kweli; hii ndiyo shabaha pekee ambayo watu wote wanafaa kufuatilia.

Mamlaka ya Muumba Hayawekewi Mipaka ya Muda, Nafasi, au Jiografia, na Mamlaka ya Muumba Yanazidi Hesabu

Hebu tutazame Mwanzo 22:17-18. Hili ni fungu jingine lililozungumziwa na Yehova Mungu, Alisema kwa Ibrahimu, “Kuwa katika kubariki nitakupa baraka, na katika kuzidisha uzao wako nitazidisha mithili ya nyota za mbinguni, na mithili ya mchanga uliopo kwenye ukanda wa pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa maadui zao; Na kupitia uzao wako kila taifa la dunia litabarikiwa; kwa kuwa umeitumikia sauti yangu.” Yehova Mungu alimbariki Ibrahimu mara nyingi ili uzao wake uweze kuzidishwa—na kuzidishwa hadi kiwango gani? Hadi kiwango kilichozungumziwa katika Maandiko: “kama nyota za mbinguni na mchanga ulio pwani.” Hii ni kusema kwamba Mungu alipenda kumpa Ibrahimu uzao uliokuwa mwingi kama nyota za mbinguni, na tele kama mchanga wa pwani. Mungu aliongea akitumia taswira, na kutoka kwenye taswira hii si vigumu kuona kwamba Mungu asingempa tu Ibrahimu uzao elfu moja, mbili, au hata elfu nyingi, lakini idadi isiyohesabika, iliyotosha kuwa uzao wa mataifa mengi ya dunia, kwani Mungu alimwahidi Ibrahimu kuwa atakuwa baba wa mataifa mengi. Na je, idadi hiyo iliamuliwa na binadamu au iliamuliwa na Mungu? Je, binadamu anaweza kudhibiti uzao kiasi gani atakaokuwa nao? Je, inategemea yeye? Haitegemei binadamu kujua kama atakuwa na uzao mbalimbali au la, sikwambii uzao mwingi kama “nyota za mbinguni, na mithili ya mchanga uliopo kwenye ukanda wa pwani.” Ni nani asiyetamani uzao wake kuwa mwingi kama nyota? Kwa bahati mbaya mambo huwa hayaendi namna unavyotaka. Licha ya vile mwanadamu anaweza kuwa na mbinu au kuweza kufanya jambo fulani, haitegemei binadamu; hakuna anayeweza kusimama nje ya kile ambacho kimeamriwa na Mungu. Kiasi ambacho Atakuruhusu, hicho ndicho utakachokuwa nacho: Kama Mungu atakupa kidogo, basi hutawahi kuwa na kingi, na kama Mungu Atakupa kingi haina faida wewe kuchukia kingi hicho ulichonacho. Je, hayo si kweli? Haya yote yanategemea Mungu, si binadamu! Binadamu hutawaliwa na Mungu, na hakuna yule anayeachwa!

Wakati Mungu alisema “uzao wako nitazidisha mithili,” hili lilikuwa agano ambalo Mungu alianzisha na Ibrahimu, sawa na agano la upinde wa mvua, lingeweza kutimizwa milele hadi milele, na pia ilikuwa ahadi iliyotolewa na Mungu kwa Ibrahimu. Mungu pekee ndiye anayefuzu na kuweza kufanya ahadi hii kutimia. Bila kujali kama binadamu anaisadiki au la, bila kujali

kama binadamu aikubali au la, na bila kujali namna binadamu anavyoitazama, na namna anavyoichukulia, haya yote yataweza kutimizwa, hadi mwisho wa maelezo ya agano hili, kulingana na matamshi yaliyotamkwa na Mungu. Matamshi ya Mungu hayatabadilishwa kwa sababu ya mabadiliko katika mapenzi au dhana za binadamu, na hayatabadilishwa kwa sababu ya mabadiliko ndani ya mtu yeyote, kitu au kifaa. Viumbe vyote vitaweza kutoweka lakini matamshi ya Mungu yatabaki milele hadi milele. Kinyume cha mambo ni, siku ambapo viumbe vyote vitatoweka ndiyo siku ile ile ambayo matamshi ya Mungu yataweza kutimizwa kabisa, kwani Yeye ndiye Muumba, na Anamiliki mamlaka ya Muumba, na nguvu za Muumba, na Anadhibiti vitu na viumbe vyote na nguvu zote za maisha; na Anaweza kusababisha kitu kutoka kule kusikokuwa na kitu, au kitu kuwa kile kisichokuwepo, na Anadhibiti mabadiliko ya viumbe vyote vilivyo na uhai na vile vilivyokufa, na kwa hivyo kwake Mungu, hakuna kinachokuwa rahisi kuliko kuzidisha uzao wa mtu. Haya yote yanaonekana ya kufikiria tu akilini mwa binadamu, sawa na hadithi za uwongo, lakini kwa Mungu, kile Anachoamua kufanya, na kuahidi kufanya, si cha kufikiria tu akilini wala si hadithi za uwongo. Badala yake ni hoja ambayo Mungu tayari ameiona, na ambayo kwa kweli itaweza kutimizwa. Je, unashukuru kuyasikia haya? Je, hoja hizi zinathibitisha kwamba uzao wa Ibrahim ulikuwa mwingi? Na ulikuwa mwingi kiasi kipi? Mwingi kiasi cha “nyota za mbinguni, na mithili ya mchanga uliopo kwenye ukanda wa pwani” kama ilivyosemwa na Mungu? Je, uliweza kuenea kotekote katika mataifa na maeneo, kwenye kila sehemu ya ulimwengu? Na ni nini kilichotimiza hoja hii? Iliweza kutimizwa kutokana na mamlaka ya matamshi ya Mungu? Kwa miaka kadhaa ifikayo mamia au elfu baada ya matamshi ya Mungu kutamkwa, matamshi ya Mungu yaliendelea kutimizwa, na bila kusita yakaendelea kuwa hoja; huu ndio uwezo wa matamshi ya Mungu, na ithubati ya mamlaka ya Mungu. Wakati Mungu alipoumba viumbe vyote hapo mwanzo, Mungu alisema na hebu kuwe na nuru, na kukawa na nuru. Tokeo hili lilifanyika haraka sana, lilitimizwa kwa muda mfupi sana, na hakukuwa na kuchelewa kokote kuhusu kukamilika na kutimizwa kwake; athari za matamshi ya Mungu zilitokea papo hapo. Vyote vilikuwa onyesho la mamlaka ya Mungu, lakini wakati Mungu alipombariki Ibrahim, Aliruhusu binadamu kuuona upande mwingine wa mamlaka ya Mungu, na Akaruhusu binadamu kuona mamlaka ya Muumba yasiyokadirika, na zaidi, Akaruhusu binadamu kuona upande halisi, bora zaidi wa mamlaka ya Muumba.

Punde tu matamshi ya Mungu yanapotamkwa, mamlaka ya Mungu yanachukua usukani wa kazi hii, na hoja iliyoahidiwa kwa kinywa cha Mungu kwa utaratibu huanza kugeuka na kuwa uhalisi. Miongoni mwa viumbe vyote, mabadiliko huanza kufanyika katika kila kitu kutokana na hayo, sawa na vile, kwenye mwanzo wa msimu wa mchipuko, nyasi hugeuka kuwa kijani, maua huchanua, macho ya maua yanachanua kutoka mitini, ndege wanaanza kuimba, nao batabukini wanaanza kurejea, nayo mashamba yanaanza kujaa watu.... Wakati wa msimu wa machipuko

unapowadia viumbe vyote hupata nguvu, na hiki ndicho kitendo cha miujiza cha Muumba. Wakati Mungu anapokamilisha ahadi zake, viumbe vyote mbinguni na ardhini vinapata nguvu mpya na kubadilika kulingana na fikira za Mungu—na hakuna kiumbe ambacho kinaachwa. Wakati kujitolea au kuahidi kunapotamkwa kutoka kwa Mungu, viumbe vyote vinatimiza wajibu wake, na vinashughulikiwa kwa minajili ya kutimizwa kwake, na viumbe vyote vinaundwa na kupangiliwa chini ya utawala wa Mungu, na vinaendeleza wajibu wao maalum, na kuhudumu kazi zao husika. Haya ndiyo maonyesho ya mamlaka ya Muumba. Unaona nini katika mambo haya? Unajuaje mamlaka ya Mungu? Kunao upana wa mamlaka ya Mungu? Kuna kipimo cha muda? Je, inaweza kusemekana kuwa na kimo fulani, au urefu fulani? Je, inaweza kusemekana kuwa na ukubwa au nguvu fulani? Je, inaweza kupimwa kwa vipimo vya binadamu? Mamlaka ya Mungu hayawakiwaki yakizima, hayaji yakienda, na hakuna mtu anayeweza kupima namna ambavyo mamlaka Yake yalivyo makubwa. Haijalishi ni muda gani utakaopita, wakati Mungu anabariki mtu, baraka hizi zitaendelea kuwepo, na kuendelea kwake kutadhihirisha agano la mamlaka ya Mungu yasiyokadirika, na kutaruhusu mwanadamu kutazama kule kujitokeza upya kwa nguvu za maisha zisizozimika za Muumba, mara kwa mara. Kila onyesho la mamlaka Yake ni onyesho timilifu la maneno kutoka kwenye kinywa Chake, na linaonyeshwa kwa vitu vyote, na kwa mwanadamu. Zaidi ya hayo, kila kitu kinachokamilishwa na mamlaka Yake ni bora zaidi ya kulinganishwa, na hakina dosari kamwe. Yaweza kusemekana kwamba fikira Zake, matamshi Yake, mamlaka Yake, na kazi zote Anazozikamilisha, zote ni picha nzuri isiyolinganishwa, na kwa viumbe, lugha ya binadamu haiwezi kuelezea umuhimu na thamani yake. Mungu anapotoa ahadi kwa mtu, haijalishi kama ni kuhusiana na pale wanakoishi, au kile wanachofanya, asili yao kabla na baada ya kupata ahadi, au hata ni vipi ambavyo mageuzi makubwa yamekuwa makubwa katika harakati zao za kuishi kwenye mazingira yao—haya yote yanajulikana kwa Mungu kama sehemu ya nyuma ya mkono Wake. Haijalishi ni muda upi umepita baada ya matamshi ya Mungu kutamkwa, kwake Yeye, ni kama vile ndio mwanzo yametamkwa. Hivi ni kusema kwamba Mungu anazo nguvu, na Anayo mamlaka kama hayo, kiasi cha kwamba Anaweza kufuatilia, kudhibiti, na kutambua kila ahadi Anayotoa kwa mwanadamu, haijalishi ahadi hiyo ni nini, haijalishi ni muda gani itachukua kutimizwa kikamilifu, na, zaidi, haijalishi upana wa sehemu ambazo kukamilika huko kunagusia—kwa mfano, muda, jiografia, kabila, na kadhalika—ahadi hii itakamilishwa, na kutambuliwa, na, zaidi, kukamilishwa kwake na kutambuliwa kwake hakutahitaji jitihada Zake hata kidogo. Na haya yanathibitisha nini? Kwamba upana wa mamlaka ya Mungu na nguvu vinatosha kudhibiti ulimwengu mzima, na wanadamu wote. Mungu aliumba nuru, lakini hiyo haimaanishi kuwa Mungu anasimamia tu nuru, kwamba Yeye anasimamia maji tu kwa sababu Aliyaumba maji, na kwamba kila kitu kingine hakina uhusiano na Mungu. Je, hii siyo suitafahamu? Ingawa baraka za Mungu kwa Ibrahimu zilikuwa zimefifia polepole kutoka kwenye kumbukumbu ya binadamu baada ya miaka

mia kadhaa, kwake Mungu, ahadi hii ilibaki vilevile. Ilikuwa kwenye mchakato wa kukamilishwa, na haikuwahi kusitishwa. Binadamu hakuwahi kujua au kusikia namna ambavyo Mungu alisisitiza mamlaka Yake, namna ambavyo vitu vyote vilivyoundwa na kupangiliwa, na ni hadithi ngapi za ajabu zilifanyika miongoni mwa vitu vyote vya uumbaji wa Mungu kwenye kipindi hiki cha muda, lakini kila kipande kizuri cha onyesho la mamlaka ya Mungu na ufunuo wa matendo Yake vilipitishwa na kutukuzwa miongoni mwa viumbe vyote, viumbe vyote vilijitokeza na kuongea kuhusu vitendo vya kimiujiza vya Muumba, na kila mojawapo ya hadithi iliyosimuliwa sana kuhusu ukuu wa Muumba juu ya viumbe vyote itaweza kutangazwa na viumbe vyote daima dawamu. Mamlaka ambayo Mungu anatawala viumbe vyote, na nguvu za Mungu, vinaonyesha viumbe vyote kwamba Mungu anapatikana kila pahali wakati wote. Wakati unashuhudia upekee wa mamlaka na nguvu za Mungu, utaona kwamba Mungu anapatikana kila mahali na nyakati zote. Mamlaka na nguvu za Mungu haviwekewi mipaka ya muda, jiografia, nafasi, au mtu yeyote, jambo au kitu. Upana wa mamlaka na nguvu za Mungu unazidi mawazo ya binadamu; haufikiriki kwa binadamu, hauwaziki kwa binadamu, na hautawahi kujulikana na binadamu.

Baadhi ya watu wanapenda kujijazia na kujifikiria, lakini, mawazo ya binadamu yanaweza kufikia wapi? Yanaweza kuzidi ulimwengu huu? Je, mwanadamu ana uwezo wa kujijazia na kufikiria uhalali na usahihi wa mamlaka ya Mungu? Je, kule kujijazia na kujifikiria kwa binadamu kunaweza kuruhusu yeye kufikia maarifa ya mamlaka ya Mungu? Vinaweza kufanya binadamu kushukuru kwa kweli na kunyenyekea mbele ya mamlaka ya Mungu? Hoja zinathibitisha kwamba uingiliaji kati na kufikiria kwa binadamu ni zao tu la akili za binadamu, na hakutoi hata msaada kidogo au manufaa kidogo kwa maarifa ya binadamu kuhusu mamlaka ya Mungu. Baada ya kusoma makala ya kidhahania ya kisayansi, baadhi wanaweza kufikiria mwezi, na vile nyota zilivyo. Ihali hii haimanishi kwamba binadamu anao ufahamu wowote wa mamlaka ya Mungu. Kufikiria kwa binadamu ni huku tu: kufikiria. Kuhusiana na hoja za mambo haya, hivi ni kusema kwamba, kwa kurejelea muunganiko wao kwa mamlaka ya Mungu, hana ung'amuzi wowote. Na je, ikiwa umeenda hadi mwezini? Je, hii inaonyesha kuwa unao ufahamu wa pande nyingi kuhusu mamlaka ya Mungu? Je, inaonyesha kwamba wewe unaweza kufikiria upana wa mamlaka na nguvu za Mungu? Kwa sababu huko kuingilia kati na kufikiria kwa mwanadamu hakuwezi kumruhusu kujua mamlaka ya Mungu, je, binadamu anafaa kufanya nini? Chaguo lenye hekima zaidi ni kutojijazia au kutojifikiria, ambapo ni kusema kwamba binadamu asiwahi kutegemea kufikiria na kutegemea uingiliaji kati inapohusu kujua mamlaka ya Mungu. Ni nini ambacho Ningependa kukwambia hapa? Maarifa ya mamlaka ya Mungu, nguvu za Mungu, utambulisho binafsi wa Mungu, na hali halisi ya Mungu haviwezi kutimizwa kwa kutegemea kufikiria kwako. Kwa vile huwezi kutegemea kufikiria ili kujua mamlaka ya Mungu,

basi ni kwa njia gani unaweza kutimiza maarifa ya kweli ya mamlaka ya Mungu? Kwa kula na kunywa maneno ya Mungu, kupitia ushirika, na kupitia kwa uzoefu wa maneno ya Mungu, utaweza kuwa na hali halisi ya kujua kwa utaratibu na uthibitishaji wa mamlaka ya Mungu na hivyo basi utafaidi kuelewa kwa utaratibu na maarifa yaliyoongezeka. Hii ndiyo njia tu ya kutimiza maarifa ya mamlaka ya Mungu; hakuna njia za mkato. Kukuuliza kutofikiria si sawa na kukufanya uketi kimyakimya ukisubiri maangamizo, au kukusitisha dhidi ya kufanya kitu. Kutotumia akili zako kuwaza na kufikiria kunamaanisha kutotumia mantiki ya kujijazia, kutotumia maarifa kuchambua, kutotumia sayansi kama msingi, lakini badala yake kufurahia, kuhakikisha, na kuthibitisha kuwa Mungu unayemsadiki anayo mamlaka, kuthibitisha kwamba Yeye anashikilia ukuu juu ya hatima yako, na kwamba nguvu Zake nyakati zote zinathibitisha kuwa Yeye Mungu Mwenyewe ni wa kweli, kupitia kwa matamshi ya Mungu, kupitia ukweli, kupitia kwa kila kitu unachokabiliana nacho maishani. Hii ndiyo njia pekee ambayo mtu yeyote anaweza kutimiza ufahamu wa Mungu. Baadhi ya watu husema kwamba wangependa kupata njia rahisi ya kutimiza nia hii, lakini unaweza kufikiria kuhusu njia kama hiyo? Nakwambia, hakuna haja ya kufikiria: Hakuna njia nyingine! Njia ya pekee ni kujua kwa uangalifu na bila kusita na kuhakikisha kile Mungu anacho na alichokupitia kwa kila neno Analolielezea na Analolifanya. Hii ndiyo njia pekee ya kujua Mungu. Kwani kile Mungu anacho na alichokupitia kwa kila kitu cha Mungu, si cha wazi na tupu—lakini cha kweli.

Hoja ya Udhhibiti wa Muumba na Utawala Juu ya Vitu Vyote na Viumbe Vilivyo Hai Inazungumzia Uwepo wa Kweli wa Mamlaka ya Muumba

Vilevile, baraka za Yehova kwa Ayubu zimerekodiwa katika Kitabu cha Ayubu. Ni nini ambacho Mungu alimpa Ayubu? “Kwa hivyo Yehova akabariki mwisho wa baadaye wa Ayubu zaidi kuliko mwanzo wake: kwa sababu alikuwa na kondoo elfu kumi na nne, na ngamia elfu sita, na elfu moja ya jozi za ng’ombe, na elfu moja ya punda wa kike” (Ayubu 42:12). Kutoka kwenye mtazamo wa binadamu, ni vitu gani alivyopewa Ayubu? Je, vilikuwa rasilimali ya binadamu? Akiwa na rasilimali hizi, je, Ayubu angeweza kuwa tajiri sana kwenye kipindi hicho? Na aliwezaje kumiliki rasilimali kama hizo? Ni nini kilisababisha utajiri wake? Bila shaka ilikuwa ni shukrani kwa baraka ya Mungu ambapo Ayubu alifanikiwa kumiliki. Namna ambavyo Ayubu alitazama rasilimali hizi, na vipi alivyochukulia baraka za Mungu, si jambo ambalo tutalizungumzia hapa. Tunapokuja katika baraka za Mungu watu wote hutamani, mchana na usiku, kubarikiwa na Mungu, ilhali binadamu hana udhibiti wowote kuhusiana na idadi ngapi ya rasilimali anaweza kufaidi katika maisha yake yote, au kama anaweza kupokea baraka kutoka kwa Mungu—na hii ni hoja isiyopingika! Mungu anayo mamlaka, na nguvu za kumpatia mwanadamu rasilimali yoyote, kumruhusu binadamu kupata tamko lolote la baraka, ilhali kuna kanuni ya baraka za Mungu. Ni aina gani ya watu ambao Mungu hubariki? Watu Anaowapenda,

bila shaka! Ibrahimu na Ayubu walibarikiwa wote na Mungu, ilhali baraka walizopokea hazikuwa sawa. Mungu alibariki Ibrahimu kwa vizazi vingi kama mchanga na nyota. Wakati Mungu alipombariki Ibrahimu, Alisababisha vizazi vya mtu mmoja, taifa moja, kuwa na nguvu na ufanisi. Katika haya mamlaka ya Mungu yalitawala mwanadamu, ambaye alipumua pumzi za Mungu miongoni mwa viumbe vyote na viumbe vyenye uhai. Chini ya ukuu wa mamlaka ya Mungu, huyu mwanadamu aliweza kupenyeza na kuwepo kwa kasi, na ndani ya upana, ulioamuliwa na Mungu. Haswa, uwezo wa taifa hili, kima cha upanuzi, na matarajio ya maisha vyote vilikuwa sehemu ya mipangilio ya Mungu, na kanuni ya haya yote ilitokana kwa ujumla kwa ahadi ambazo Mungu alimpa Ibrahimu. Hivi ni kusema kwamba, licha ya hali zozote zile, ahadi za Mungu zingeendelea mbele bila kizuizi na kuweza kutambuliwa kulingana na uwepo wa mamlaka ya Mungu. Katika ahadi ambayo Mungu alimpa Ibrahimu, licha ya misukosuko ya ulimwengu, licha ya umri, licha ya majanga yanayovumiliwa na mwanadamu, vizazi vya Ibrahimu visingeweza kukabiliwa na hatari ya maangamizo, na taifa lao lisingefifia na kutokomea. Baraka ya Mungu kwa Ayubu, hata hivyo, ilimfanya kuwa tajiri wa kupindukia. Kile Mungu alichompa kilikuwa mseto wa viumbe hai, vinavyopumua, maelezo yake yalikuwa—idadi yao, kasi yao ya kuzaa, kima cha kuishi, kiwango cha mafuta kwenye viumbe hivyo, na kadhalika—vilidhibitiwa pia na Mungu. Ingawa viumbe hivi hai havikumiliki uwezo wa kuongea, navyo pia vilikuwa sehemu ya mipangilio ya Muumba, na kanuni za mipangilio ya Mungu zilikuwa kulingana na baraka ambayo Mungu aliahidi Ayubu. Katika baraka ambazo Mungu alimpa Ibrahimu na Ayubu, Ingawa kile kilichokuwa kimeahidiwa kilikuwa tofauti, mamlaka ambayo Muumba alitumia kutawala viumbe vyote na viumbe vilivyo na uhai yalikuwa yale yale. Kila maelezo ya mamlaka na Nguvu za Mungu yameonyeshwa kwenye ahadi Zake tofauti na baraka zake kwa Ibrahimu na Ayubu, kwa mara nyingine zaonyesha binadamu kwamba mamlaka ya Mungu ni zaidi ya kufikiria kwa binadamu. Maelezo haya yanamwambia binadamu kwa mara nyingine kwamba kama angetaka kujua mamlaka ya Mungu, basi hii itawezekana tu kupitia kwa maneno ya Mungu na kuweza kupitia kazi ya Mungu.

Mamlaka ya Mungu ya ukuu juu ya viumbe vyote huruhusu binadamu kuweza kuona ukweli kwamba: Mamlaka ya Mungu hayapo tu katika matamshi “Mungu akasema, na Kuwepo na nuru, na kukawa na nuru, na, Kuwepo na anga, na kukawa na anga, na, Kuwepo na ardhi, na kukawa na ardhi,” lakini, vilevile namna Alivyofanya nuru ile kuendelea kuwepo, kulizuia anga dhidi ya kutoweka na Akaiweka ardhi milele ikiwa kando na maji, pamoja na maelezo ya namna Alivyotawala na kusimamia viumbe: nuru, anga, na ardhi. Nini kingine unachoona katika baraka za Mungu kwa mwanadamu? Ni wazi, kwamba baada ya Mungu kuwabariki Ibrahimu na Ayubu, nyayo za Mungu hazikusita, kwani Alikuwa tu ameanza kuonyesha mamlaka Yake, na Alinuia kuhakikisha kwamba kila mojawapo ya matamshi Yake yangekuwa uhalisia, na

kuhakikisha kuwa kila mojawapo ya maelezo ambayo Alizungumza yanatokea kuwa kweli, na kwa hivyo kwenye miaka iliyofuata, Aliendelea kufanya kila kitu Alichonulia. Kwa sababu Mungu anayo mamlaka, pengine inaonekana kwa binadamu kwamba Mungu huongea tu, na Hahitaji kuinua hata kidole chake ili mambo yote yaweze kutimizwa. Kufikiria hivyo, ni, lazima Niseme, mzaha! Kama utachukua mtazamo wa upande mmoja wa Mungu kuanzisha agano na binadamu kwa kutumia maneno, na ukamilishaji wa kila kitu na Mungu kwa kutumia maneno, na huwezi kuona ishara na hoja mbalimbali ambazo mamlaka ya Mungu yanatawala juu ya kila kitu, basi ufahamu wako kuhusiana na mamlaka ya Mungu ni mdogo mno na wa mzaha! Kama binadamu anafikiria Mungu kuwa hivyo, basi, lazima isemwe, maarifa ya binadamu kuhusu Mungu yameendeshwa hadi kwenye shimo la mwisho, na sasa yamefika mwisho wenyewe, kwani Yule Mungu ambaye binadamu anafikiria kuhusu ni mashine tu ya kutoa amri, na si Mungu anayemiliki mamlaka. Je, umeona nini kupitia kwenye mifano ya Ibrahimu na Ayubu? Je, umeuona upande halisia wa mamlaka na nguvu za Mungu? Baada ya Mungu kuwabariki Ibrahimu na Ayubu, Mungu hakubakia mahali Alipokuwa, wala Yeye kuwaweka wajumbe Wake kazini huku Akisubiri kuona matokeo yake yatakuwa yapi. Kinyume cha mambo ni kuwa, pindi Mungu alipotamka maneno Yake, akiongozwa na mamlaka ya Mungu, mambo yote yalianza kukubaliana na kazi ambayo Mungu alinulia kufanya, na kulikuwepo na watu waliokuwa wamejitayarisha, vitu, na vifaa ambavyo Mungu alihitaji. Hivi ni kusema kwamba, punde tu maneno hayo yalipotamkwa kutoka kwenye kinywa cha Mungu, mamlaka ya Mungu yalianza kutumika kotekote kwenye ardhi nzima, na Akaweka wazi mkondo ili kuweza kukamilisha na kutimiza ahadi Alizotoa kwa Ibrahimu na Ayubu, huku Akifanya pia mipango na matayarisho yote kuhusiana na kila kitu kilichohitajika kwa kila awamu Aliyopanga kutekeleza. Kwa wakati huu, hakuwashawishi tu wafanyakazi Wake, lakini pia na viumbe vyote vilivyokuwa vimeumbwa na Yeye. Hivyo ni kusema kwamba upana ambao mamlaka ya Mungu yalitiliwa maanani haukujumuisha tu wajumbe, lakini, vilevile, vitu vyote, vilivyoshawishiwa ili kutii ile kazi ambayo Alinulia kukamilisha; hizi ndizo zilizokuwa tabia mahususi ambazo mamlaka ya Mungu yalitumiwa. Katika kufikiria kwako, baadhi ya watu wanaweza kuwa na ufahamu ufuatao kuhusiana na mamlaka ya Mungu: Mungu anayo mamlaka, na Mungu anao uwezo, na hivyo basi Mungu anahitaji kubaki katika mbingu ya tatu, au Anahitajika tu kubakia mahali maalum, na hahitajiki kufanya kazi yoyote fulani, na uzima wa kazi ya Mungu unakamilishwa katika fikira Zake. Baadhi wanaweza kusadiki kuwa, Ingawa Mungu alibariki Ibrahimu, Mungu hakuhitajika kufanya kitu chochote, na ilitosha kwake Yeye kutamka tu matamshi Yake. Je, hivi ndivyo ilivyofanyika kweli? Bila shaka la! Ingawa Mungu anamiliki mamlaka na nguvu, mamlaka Yake ni ya kweli na halisia, si matupu. Uhalisi na ukweli wa mamlaka ya Mungu na nguvu hufichuliwa kwa utaratibu, kuwekwa ndani ya uumbaji Wake wa vitu vyote, na udhibiti wa vitu vyote, na katika mchakato ambao Anaongoza na kusimamia wanadamu. Kila mbinu, kila

mtazamo na kila maelezo ya ukuu wa Mungu juu ya wanadamu na vitu vyote, na kazi yote ambayo Amekamilisha, vilevile ufahamu Wake kuhusu vitu vyovyote—vinathibitisha kwa kweli kwamba mamlaka na nguvu za Mungu si maneno matupu. Mamlaka na nguvu Zake vyote vinaonyeshwa na kufichuliwa kila mara, na katika mambo yote. Maonyesho haya na ufunuo vyote vinazungumzia uwepo wa halisi wa mamlaka ya Mungu, kwani Yeye ndiye anayetumia mamlaka na nguvu Zake kuendeleza kazi Yake, na kuamuru vitu vyote, na kutawala vitu vyote kila wakati, na nguvu na mamlaka Yake, vyote haviwezi kubadilishwa na malaika, au wajumbe wa Mungu. Mungu aliamua ni baraka gani Angempa Ibrahimu na Ayubu—uamuzi ulikuwa wa Mungu. Hata Ingawa wajumbe wa Mungu waliweza kumtembelea Ibrahimu na Ayubu wao binafsi, vitendo vyao vilikuwa kulingana na amri za Mungu, na kulingana na mamlaka ya Mungu, na pia walikuwa wakifuata ukuu wa Mungu. Ingawa binadamu anawaona wajumbe wa Mungu wakimtembelea Ibrahimu, na hashuhudii Yehova Mungu binafsi akifanya chochote kwenye rekodi za Biblia, kwa hakika Yule Mmoja tu ambaye anatilia mkazo nguvu na mamlaka ni Mungu Mwenyewe, na hali hii haivumilii shaka yoyote kutoka kwa binadamu yeyote! Ingawa umewaona malaika na wajumbe wakimiliki nguvu nyingi, na wametenda miujiza, au wamefanya baadhi ya mambo yaliyoagizwa na Mungu, vitendo vyao ni kwa minajili tu ya kukamilisha agizo la Mungu, na wala si tu kuonyesha mamlaka ya Mungu—kwani hakuna binadamu au kifaa kilicho na, au kinachomiliki, mamlaka ya Muumba ya kuumba vitu vyote na kutawala vitu vyote. Na kwa hivyo hakuna binadamu au kifaa chochote kinaweza kutumia au kuonyesha mamlaka ya Muumba.

Mamlaka ya Muumba Hayabadiliki na ni Yasiyokosewa

Ni nini umeona katika sehemu hizi tatu za maandiko? Je, umeona kuwa kuna kanuni ambayo Mungu hutumia mamlaka Yake? Kwa mfano, Mungu aliutumia upinde wa mvua kuanzisha agano na binadamu, ambapo Aliuweka upinde wa mvua katika mawingu ili kumwambia binadamu kuwa Yeye Hatawahi tena kutumia gharika kuangamiza ulimwengu. Je, upinde wa mvua tunaouona leo, bado ndio uleule uliozungumziwa kutoka kwenye kinywa cha Mungu? Je, asili na maana yake vimebadilika? Bila shaka, havijabadilika. Mungu alitumia mamlaka Yake ili kutekeleza kitendo hiki, nalo agano Aliloanzisha na binadamu limeendelea hadi leo, na muda ambao agano hili litabadilishwa, bila shaka, ni uamuzi wa Mungu. Baada ya Mungu kutamka “Mimi nauweka upinde wangu wa mvua mawinguni,” siku zote Mungu alifuata agano hili, Alilifuata hadi leo. Unaona nini katika haya? Ingawa Mungu anayamiliki mamlaka na nguvu, Anayo bidii sana na Anafuata kanuni katika vitendo Vyake, na Anashikilia maneno Yake. Bidii Yake na kanuni za vitendo Vyake, vinaonyesha namna Muumba asivyoweza kukosewa na namna ambavyo mamlaka ya Muumba yalivyo magumu kushindwa. Ingawa Anamiliki mamlaka ya juu, na kila kitu kinatawaliwa na Yeye, na japokuwa Anazo nguvu za kutawala vitu vyote,

Mungu hajawahi kuharibu mpango Wake au kutatiza mpangilio Wake mwenyewe, na kila wakati Anapotumia mamlaka Yake, ni kulingana na umakinifu unaohitajika kwenye kanuni Zake mwenyewe na hasa kwa kufuata kile kilichotamkwa kutoka kwenye kinywa Chake, na kufuata hatua na majukumu ya mpango Wake. Sina haja ya kusema kwamba kila kitu kinachotawaliwa na Mungu pia kinatii kanuni ambazo mamlaka ya Mungu yanatumika, na hakuna mwanadamu au kitu kisichojumuishwa kwenye mipangilio ya mamlaka Yake, wala hakuna anayeweza kubadilisha kanuni ambazo mamlaka Yake yanatumika. Kwenye macho ya Mungu, wale wanaobarikiwa hupokea utajiri mzuri unaoletwa na mamlaka Yake, na wale wanaolaaniwa hupokea adhabu yao kwa sababu ya mamlaka ya Mungu. Chini ya ukuu wa mamlaka ya Mungu, hakuna binadamu au kitu ambacho hakijumuishwi, kwenye utumiaji wa mamlaka Yake, wala hakuna kinachoweza kubadilisha kanuni hizi ambazo mamlaka Yake yanatumiwa. Mamlaka ya Muumba hayabadilishwi kwa mabadiliko ya aina yoyote ile, na, vilevile, kanuni ambazo mamlaka Yake yanatumiwa hazibadiliki kwa sababu yoyote ile. Mbingu na ardhi vyote vinaweza kupitia misukosuko mingi, lakini mamlaka ya Muumba hayatabadilika; vitu vyote vitatoweka, lakini mamlaka ya Muumba hayatawahi kutoweka. Hiki ndicho kiini cha mamlaka ya Muumba ambayo hayabadiliki na ni yasiyokosewa, na huu ndio upekee wenyewe wa Muumba!

Maneno yaliyo hapa chini ni lazima katika kujua mamlaka ya Mungu, na maana yake yametolewa kwenye ushirika ulio hapa chini. Hebu tuendelee kuyasoma Maandiko.

4. Amri ya Mungu kwa Shetani

Ayubu 2:6 Naye Yehova akasema kwa Shetani, Tazama, yeye yuko katika mkono wako; lakini uuhifadhi uhai wake.

Shetani Hajawahi Kuthubutu Kukiuka Mamlaka ya Muumba, na Kwa Sababu Hiyo, Vitu Vyote Vinaishi kwa Mpangilio

Hili ni dondoo kutoka katika Kitabu cha Ayubu, na “yeye” katika maneno haya inaashiria Ayubu. Ingawa imeandikwa kwa muhtasari, sentensi hii inaelezea masuala mengi. Inafafanua mabadilishano fulani kati ya Mungu na Shetani kwenye ulimwengu wa kiroho, na inatwambia kuwa kiini cha maneno ya Mungu kilikuwa Shetani. Pia inarekodi kile kilichozungumziwa mahususi na Mungu. Maneno ya Mungu yalikuwa amri na shurutisho kwa Shetani. Maelezo mahususi ya shurutisho hili ni kuhusiana na kuyaokoa maisha ya Ayubu na pale ambapo Mungu aliweka masharti namna ambavyo Shetani alifaa kumshughulikia Ayubu—Shetani alilazimika kuyaokoa maisha ya Ayubu. Kitu cha kwanza tunachojifunza kutoka kwenye sentensi hii ni kwamba matamshi haya yalitamkwa na Mungu kwa Shetani. Kulingana na maandishi ya asili ya Kitabu cha Ayubu, yanatwambia usuli wa matamshi kama hayo: Shetani alipenda kumshutumu

Ayubu, na hivyo lazima angepokea huo mkataba wa Mungu kabla hajamtia majaribuni. Wakati alipokubali ombi la Shetani kumjaribu Ayubu, Mungu aliweza kumtaja Shetani sharti lifuatalo: “Ayubu yuko mkononi mwako; lakini uuhifadhi uhai wake.” Ni nini asili ya maneno haya? Ni wazi kwamba ni amri, ni shurutisho. Baada ya kuelewa asili ya maneno haya, unafaa, bila shaka, pia kung’amua kwamba Aliyetoa shurutisho hili ni Mungu, na kwamba aliyepokea amri hii, na akaitii, ni Shetani. Sina haja ya kusema kwamba katika shurutisho hili, uhusiano kati ya Mungu na Shetani uko wazi kwa yeyote ambaye anasoma maneno haya. Bila shaka, huu ndio uhusiano kati ya Mungu na Shetani katika ulimwengu wa kiroho, na tofauti kati ya utambulisho na hadhi ya Mungu na Shetani, iliyoelezwa kwenye rekodi za mabadilishano ya mazungumzo ya Mungu na Shetani katika Maandiko, na, hadi leo, ni mfano mahususi na rekodi ya maandishi ambapo binadamu anaweza kujifunza tofauti kuu kati ya utambulisho na hadhi ya Mungu na Shetani. Wakati huu, lazima Niseme kwamba, rekodi ya maneno haya ni waraka muhimu sana katika ufahamu wa binadamu juu ya hadhi na utambulisho wa Mungu, na inatoa taarifa muhimu kwa maarifa ya mwanadamu kuhusu Mungu. Kupitia mabadilishano haya ya Mungu na Shetani katika ulimwengu wa kiroho, binadamu anaweza kuelewa dhana moja mahususi katika mamlaka ya Muumba. Maneno haya ni ushuhuda mwingine wa kuonyesha mamlaka ya kipekee ya Muumba.

Kwa nje, Yehova Mungu yuko katika mazungumzo na Shetani. Kwa kuzingatia kiini, mtazamo ambao Yehova Mungu anaongea, na nafasi ambayo ambamo Anasimama ni ya juu zaidi kuliko ya Shetani. Hivi ni kusema kwamba Yehova Mungu anamwamuru Shetani na sauti ya kushurutisha, na Anamwambia Shetani ni nini anafaa afanye na kile hafai kufanya, kwamba tayari Ayubu yu mikononi mwake, na yuko huru kumfanya Ayubu vyovyote atakavyo—lakini asiyachukue maisha ya Ayubu. Ujumbe hapa ni, Ingawa Ayubu alikuwa amewekwa kwenye mikono ya Shetani, maisha yake hayakuchukuliwa na Shetani; hakuna anayeweza kuchukua maisha ya Ayubu kutoka mikononi mwa Mungu isipokuwa Mungu amruhusu. Mtazamo wa Mungu unafafanuliwa waziwazi katika amri hii kwa Shetani, na amri hii pia inajionyesha na kufichua msimamo ambao Yehova Mungu anazungumza na Shetani. Katika haya, Yehova Mungu hashikilii tu hadhi ya Mungu aliyeumba nuru, na hewa, na vitu vyote na viumbe hai, au ya Mungu anayeshikilia ukuu juu ya vitu vyote na viumbe hai, lakini pia ya Mungu ambaye anaamuru mwanadamu, na kuamuru Jahanamu, Mungu ambaye anadhibiti maisha na kifo cha viumbe vyote hai. Katika ulimwengu wa kiroho, ni nani mbali na Mungu ambaye angethubutu kutoa shurutisho kama hilo kwa Shetani? Na ni kwa nini Mungu binafsi Alitoa shurutisho Lake kwa Shetani? Kwa sababu maisha ya binadamu, pamoja na yale ya Ayubu, yanadhibitiwa na Mungu. Mungu hakumruhusu Shetani kujeruhi au kuchukua maisha ya Ayubu, hivyo ni kusema kwamba kabla ya Mungu kumruhusu Shetani kumjaribu Ayubu, Mungu bado alikumbuka kutoa

shurutisho maalum kama hilo, na kwa mara nyingine Akamwamuru Shetani asiyachukue maisha ya Ayubu. Shetani hajawahi kuthubutu kukiuka mamlaka ya Mungu, na, vilevile, amesikiliza kwa umakinifu siku zote na kutii shurutisho na amri mahususi za Mungu, asiwahi thubutu kuzivunja, na, bila shaka asithubutu kubadilisha kwa hiari shurutisho zozote za Mungu. Hiyo ndiyo mipaka ambayo Mungu amemwekea wazi Shetani, na hivyo Shetani hajawahi thubutu kuvuka mipaka hiyo. Huu si uwezo wa mamlaka ya Mungu? Je, huu si ushuhuda wa mamlaka ya Mungu? Wa namna ya kuwa mbele ya Mungu, na namna ya kumtazama Mungu, Shetani anao ung'amuzi bora zaidi kuliko mwanadamu, hivyo, katika ulimwengu wa kiroho, Shetani anaona hadhi na mamlaka ya Mungu vizuri sana, na anatambua sana ule uwezo wa mamlaka ya Mungu na kanuni zinazotilia mkazo kwenye mamlaka Yeye. Hathubutu, kamwe, kutozitia maanani kanuni hizo, wala hathubutu kukiuka kanuni hizo kwa vyovyote vile, au kufanya chochote ambacho kinakiuka mamlaka ya Mungu, na hathubutu kukabiliana na hasira ya Mungu kwa njia yoyote. Ingawa ni mwovu na mwenye kiburi kiasili, Shetani hajawahi kuthubutu kuvuka mipaka na viwango alivyowekewa na Mungu. Kwa miaka milioni, ametii kwa umakinifu mipaka hii, ametii kila amri na shurutisho lililotolewa na Mungu na hajawahi kuthubutu kukanyaga juu ya alama. Ingawa ni mwenye kijicho, Shetani ni “mwerevu” zaidi kuliko mwanadamu aliyepotoka; anajua utambulisho wa Muumba, na anajua mipaka yake. Kutokana na vitendo vya Shetani vya kunyenyekea tunaweza kuona kwamba mamlaka na nguvu za Mungu ni maelekezo ya mbinguni ambayo hayawezi kukiukwa na Shetani, na kwamba yanatokana na upekee na mamlaka ya Mungu ndiposa viumbe vyote vinabadilika na kuzalisha katika njia ya mpangilio, kwamba mwanadamu anaweza kuishi na kuongezeka kupitia ndani ya mkondo ulioanzishwa na Mungu, huku hakuna mtu au kifaa kinachoweza kuuharibu mpango huu, na hakuna mtu au kifaa kinachoweza kubadilisha sheria hii—kwani vyote vinatoka kwenye mikono ya Muumba na kwenye mpangilio na mamlaka ya Muumba.

Mungu Pekee, Ambaye Anao Utambulisho wa Muumba, Anamiliki Mamlaka ya Kipekee

Ule utambulisho wa pekee wa Shetani umesababisha watu wengi kuonyesha shauku thabiti kwenye maonyesho yake ya dhana mbalimbali. Kunao hata watu wengi wajinga wanaosadiki kwamba, kama vile Mungu, Shetani anamiliki mamlaka, kwani Shetani anaweza kuonyesha miujiza, na anaweza kufanya mambo ambayo mwanadamu hawezi kufanya. Kwa hivyo, mbali na kumwabudu Mungu, mwanadamu pia anahifadhi nafasi kwenye moyo wake, na hata humwabudu Shetani kama Mungu. Watu hawa wote ni wa kusikitikiwa na kuchukiwa. Ni wa kusikitikiwa kwa sababu ya kutojua kwao, na wa kuchukiwa kwa sababu ya hali yao ya uasi wa kidini na hali halisi ya maovu ya ndani kwa ndani. Wakati huu Nahisi kwamba ni muhimu niwafahamishe kuhusu maana ya mamlaka, yanaashiria nini, na yanawakilisha nini. Kwa mazungumzo ya jumla, Mungu Mwenyewe ni mamlaka, mamlaka Yake yanaashiria mamlaka ya

juu na hali halisi ya Mungu, na mamlaka ya Mungu Mwenyewe yanawakilisha hadhi na utambulisho wa Mungu. Kwa hiyo, je, Shetani huthubutu kusema kwamba yeye ni Mungu? Je, Shetani huthubutu kusema kwamba aliumba viumbe vyote, na anashikilia ukuu juu ya viumbe vyote? Bila shaka la! Kwani hawezi kuumba viumbe vyote; mpaka leo, hajawahi kuumba chochote kilichoumbwa na Mungu, na hajawahi kuumba chochote kilicho na maisha. Kwa sababu hana mamlaka ya Mungu, hatawahi endapo itawezekana kumiliki hadhi na utambulisho wa Mungu, na hili linaamuliwa na hali yake halisi. Je, anazo nguvu sawa na Mungu? Bila shaka hana! Tunaita nini vitendo vya Shetani, na miujiza inayoonyeshwa na Shetani? Je, ni nguvu? Vitendo hivi vinaweza kuitwa mamlaka? Bila shaka la! Shetani huelekeza wimbi la maovu, na misukosuko, uharibifu, na kuchachawiza kila dhana ya kazi ya Mungu. Kwa miaka elfu kadhaa iliyopita, mbali na kupotosha na kunyanyasa mwanadamu, na kumjaribu na kumdanganya binadamu hadi kufikia kiwango cha uovu, na ukataaji wa Mungu, ili binadamu aweze kutembea kwenye bonde la kivuli cha mauti, je, Shetani amefanya chochote ambacho kinastahili hata kumbukumbu ndogo zaidi, pongezi au sherehe ndogo zaidi kutoka kwa binadamu? Kama Shetani angemiliki mamlaka na nguvu, je, binadamu angepotoshwa naye? Kama Shetani angemiliki mamlaka na nguvu, je, mwanadamu angepata madhara kutokana nayo? Kama Shetani angemiliki mamlaka na nguvu, je, mwanadamu angemwacha Mungu na kugeukia mauti? Kwa sababu Shetani hana mamlaka au nguvu, ni nini ambacho tunafaa kuhitimisha kuhusu hali halisi ya kila kitu anachofanya? Kunao wale wanaofafanua kila kitu ambacho Shetani hufanya kama ujanja mtupu, ilhali Nasadiki kwamba ufafanuzi kama huo haufai sana. Je, Matendo maovu ya kupotosha mwanadamu ni ujanja mtupu tu? Nguvu za maovu ambazo Shetani alimnyanyasia Ayubu, na tamania lake kali la kumnyanyasa na kumpotosha, lisingewezekana kutimizwa kupitia kwa ujanja mtupu tu. Tukiangalia nyuma, tunaona kwamba, mara moja, kondoo na ng'ombe wa Ayubu walitawanyishwa kila pahali kote kwenye milima na vilima, walikuwa hawapo tena; kwa muda mfupi tu, utajiri mwingi wa Ayubu ukatoweka. Je, yawezekana kwamba haya yote yalitimizwa kupitia kwa ujanja mtupu tu? Asili ya yale yote ambayo Shetani hufanya yanalingana na kuingiliana na istilahi mbaya kama vile kudhoofisha, kukatiza, kuharibu, kudhuru, maovu, hali ya kuwa na kijicho, na giza, na kwa hivyo matukio haya yote ambayo si ya haki na ni maovu yanahusiana na kuunganika kwenye vitendo vya Shetani, na hayawezi kutenganishwa na ile hali halisi ya uovu wa Shetani. Haijalishi ni vipi ambavyo Shetani “alivyo na nguvu”, haijalishi ni vipi Shetani alivyo mwenye kuthubutu na haijalishi ni vipi uwezo wake ulivyo mwingi katika kusababisha madhara, haijalishi ni vipi anavyotumia mbinu zenye mseto mpana ambazo zinapotosha na kudanganya binadamu, haijalishi ni vipi alivyo mwerevu kupitia kwenye ujanja na njama zake ambazo anadhalilisha binadamu, haijalishi ni vipi anavyoweza kujibadilisha katika mfumo ule aliomo, hajawahi kuweza kuumba kiumbe chochote kimoja, hajawahi kuweza kuweka wazi sheria au kanuni za uwepo wa viumbe vyote, na hajawahi

kutawala na kudhibiti kifaa chochote, kiwe ni chenye uhai au kisichokuwa na uhai. Ndani ya ulimwengu na mbingu, hakuna hata mtu au kifaa kimoja kilichotokana na Shetani, au kilichopo kwa sababu ya Shetani; hakuna hata mtu au kifaa kimoja ambacho kimetawaliwa na Shetani, au kudhibitiwa na Shetani. Kinyume cha mambo ni kwamba, hana budi kuishi katika utawala wa Mungu lakini, vilevile, lazima atii shurutisho na amri zote za Mungu. Bila ruhusa ya Mungu, ni vigumu sana kwa Shetani kugusa hata tone la maji au chembechembe ya mchanga kwenye ardhi; bila ruhusa ya Mungu, Shetani hana hata hiari ya kusongea mchwa wanaojiendea zao kwenye ardhi, sikwambii hata mwanadamu, aliyeumbwa na Mungu. Kwenye macho ya Mungu, Shetani ni duni zaidi ya yungiyungi kwenye mlima, hadi kwenye ndege wanaopaa hewani, hadi kwenye samaki walio baharini, hadi kwenye funza kwenye juu ya nchi. Wajibu wake miongoni mwa viumbe vyote ni kuhudumia viumbe vyote, na kufanyia kazi mwanadamu, na kuhudumia kazi ya Mungu na mpango Wake wa usimamizi. Licha ya vile anavyoonea wenzake kijicho katika asili yake, na vile ambavyo hali yake halisi ya maovu ilivyo, kitu ambacho Shetani anaweza kufanya tu ni kuweza kukubaliana kwa wajibu kuhusiana na kazi yake: kuwa mwenye huduma kwa Mungu, na kuwa mjalizo kwa Mungu. Hiki ndicho kiini na nafasi ya Shetani. Hali yake halisi haijaungana na maisha, haijaungana na nguvu, haijaungana na mamlaka; ni kitu cha kuchezea tu kwenye mikono ya Mungu, mtambo tu kwenye huduma ya Mungu!

Baada ya kuelewa uso wa kweli wa Shetani, watu wengi bado wangali hawajaelewa ni nini maana ya mamlaka, hivyo basi wacha Mimi nikuelezee! Mamlaka yenyewe yanaweza kufafanuliwa kama nguvu za Mungu. Kwanza, inaweza kusemekana kwa uhakika kwamba mamlaka na nguvu vyote ni vizuri. Havina uunganisho wowote na kitu chochote kibaya, na havina uhusiano wowote na viumbe vyovyote vilivyoumbwa au vile ambavyo havikuumbwa. Nguvu za Mungu zinaweza kuumba viumbe vya mfumo wowote ulio na uzima na nguvu, na haya yote yanaamuliwa na uzima wa Mungu. Mungu ni uzima, kwa hivyo Yeye ndiye chanzo cha viumbe hai vyote. Vilevile, mamlaka ya Mungu yanaweza kufanya viumbe vyote kutii kila neno la Mungu, yaani kuumbika kulingana na matamshi yanayotoka kwenye kinywa cha Mungu, na kuishi na kuzaana kwa amri ya Mungu, ambapo baadaye Mungu anatawala na kuamuru viumbe vyote hai, na hakutakuwa na kupotoka kokote, daima dawamu. Hakuna mtu au kifaa kilicho na mambo haya; Muumba tu ndiye anayemiliki na aliye na nguvu kama hizo, na hivyo basi yanaitwa mamlaka. Huu ndio upekee wa Muumba. Kwa hivyo, haijalishi kama ni neno lenyewe “mamlaka” au hali halisi ya mamlaka haya, kila mojawapo linaweza tu kuhusishwa na Muumba kwa sababu ni ishara ya utambulisho na hali halisi ya kipekee ya Muumba; na inawakilisha utambulisho na hadhi ya Muumba, mbali na Muumba, hakuna mtu au kifaa kinachoweza kuhusishwa na neno “mamlaka” Huu ni ufasiri wa mamlaka ya kipekee ya Muumba.

Ingawa Shetani alimwangalia Ayubu kwa macho ya kutamani mali yake, bila ya ruhusa ya Mungu hakuthubutu kugusa hata unywele mmoja wa mwili wa Ayubu. Ingawa ni mwenye uovu na unyama wa ndani, baada ya Mungu kutoa shurutisho Lake kwake, Shetani hakuwa na chaguo lakini kutii shurutisho la Mungu. Na kwa hivyo, hata Ingawa Shetani alionekana kana kwamba ameshikwa na kichaa sawa na mbwa-mwitu miongoni mwa kondoo alipomjia Ayubu, hakuthubutu kusahau mipaka aliyowekewa wazi na Mungu, hakuthubutu kukiuka shurutisho za Mungu, na kwa hayo yote, Shetani hakuthubutu kutoka kwenye kanuni ya maneno ya Mungu—je, hii si kweli? Kutokana na mtazamo huu wa maisha, tunaona kwamba Shetani hathubutu kuvunja matamshi yoyote yale ya Yehova Mungu. Kwake Shetani, kila neno kutoka kwenye kinywa cha Mungu ni shurutisho, na sheria ya mbinguni, na maonyesho ya mamlaka ya Mungu—kwani nyuma ya kila neno la Mungu kunadokezwa adhabu ya Mungu kwa wale wanaokiuka maagizo ya Mungu, na wale wasiotii na wanaopinga sheria za mbinguni. Shetani anajua wazi kwamba kama atakiuka shurutisho za Mungu, basi lazima akubali athari za kukiuka mamlaka ya Mungu na kupinga sheria za mbinguni. Na sasa athari hizi ni zipi? Sina haja ya kusema kwamba, athari hizi bila shaka, ni adhabu kutoka kwa Mungu. Vitendo vya Shetani kwake Ayubu vilikuwa tu mfano mdogo wa yeye kumpotosha binadamu, na wakati ambapo Shetani alipokuwa akitekeleza vitendo hivi, ile mipaka ambayo Mungu Aliweka na amri Alizotoa kwake Shetani vilikuwa tu mfano mdogo wa kanuni zinazotokana na kila kitu anachofanya. Aidha, wajibu na nafasi ya Shetani katika suala hili ulikuwa tu mfano mdogo wa wajibu na nafasi yake katika kazi ya usimamizi wa Mungu, na utiifu kamili wa Shetani kwa Mungu wakati alipomjaribu Ayubu, ulikuwa tu mfano mdogo wa namna ambavyo Shetani hakuthubutu kuweka hata upinzani mdogo kwa Mungu katika kazi ya usimamizi wa Mungu. Ni onyo gani ambalo mifano hii midogo inakupa? Miongoni mwa mambo yote, akiwemo Shetani, hakuna mtu au kitu kinachoweza kukiuka sheria na kanuni za mbinguni zilizowekwa wazi na Muumba, na hakuna mtu au kitu kinachothubutu kukiuka sheria na kanuni hizi za mbinguni, kwani hakuna mtu au kifaa kinaweza kubadilisha au kuepuka adhabu ambayo Mungu anawawekea wale wanaokosa kumtii. Ni Muumba tu anayeweza kuanzisha sheria na kanuni za mbinguni, ni Muumba tu aliye na nguvu za kuanza kuzitekeleza na nguvu za Muumba ndizo haziwezi kukiukwa na mtu au kitu chochote. Haya ndiyo mamlaka ya kipekee ya Muumba, mamlaka haya yako juu zaidi miongoni mwa mambo yote, na kwa hivyo haiwezekani kusema kwamba “Mungu ndiye mkubwa zaidi naye Shetani ni nambari mbili.” Isipokuwa Muumba anayemiliki mamlaka ya kipekee, hakuna Mungu mwingine.

Je, sasa unayo maarifa mapya kuhusu mamlaka ya Mungu? Kwanza, kunayo tofauti kati ya mamlaka ya Mungu yaliyotajwa hivi punde na nguvu za binadamu? Na tofauti ni nini? Baadhi ya wanadamu husema kwamba hakuna ulinganifu wowote kati ya haya mawili. Hayo ni kweli!

Ingawa watu husema kwamba hakuna ulinganisho kati ya haya mawili, kwenye fikira na mawazo ya binadamu, nguvu za binadamu mara nyingi zinadhaniwa kuwa mamlaka, na haya mawili hulinganishwa mara nyingi sako kwa bako. Ni nini kinachoendelea hapa? Je, si watu wanafanya kosa la kubadilisha bila ya kuwa waangalifu kitu kimoja na kingine? Vitu hivi viwili havina uhusiano wowote na hakuna ulinganisho wowote kati yavyo, ilhali watu bado hawawezi kuelewa. Je, haya yatatuliwe vipi? Kama ungependa kwa kweli kupata suluhu, njia ya pekee ni kuelewa na kujua mamlaka ya kipekee ya Mungu. Baada ya kuelewa na kujua mamlaka ya Muumba, hutataja kwa mkupuo mmoja nguvu za binadamu na mamlaka ya Mungu.

Nguvu za binadamu zinarejelea nini? Kwa ufupi, ni uwezo au mbinu inayoweza tabia potovu, matamania na malengo ya binadamu kuweza kupanuliwa au kutimizwa hadi kiwango cha juu zaidi. Je, haya yatumike kumaanisha mamlaka? Haijalishi ni vipi ambavyo malengo na matamania ya binadamu yalivyo makubwa au yenye faida, mtu huyu hawezi kusemekana amemiliki mamlaka; kama amezidi sana, haya majivuno na ufanisi ni maonyesho tu ya upumbavu wa Shetani miongoni mwa binadamu; kama imezidi sana, ni upuzi ambao Shetani anaendeleza kama babu yake mwenyewe ili kutimiza maono yake ya kuwa Mungu.

Unatazama vipi haswa mamlaka ya Mungu sasa? Kwa vile sasa maneno haya yamezungumziwa kwenye ushirika, unafaa kuwa na maarifa mapya kuhusu mamlaka ya Mungu. Na kwa hivyo Nakuuliza: Mamlaka ya Mungu yanaashiria nini? Je, yanaashiria ule utambulisho wa Mungu Mwenyewe? Je, yanaashiria nguvu za Mungu Mwenyewe? Je, yanaashiria hadhi ya kipekee ya Mungu Mwenyewe? Miongoni mwa mambo yote, ni katika kitu gani umeona mamlaka ya Mungu? Uliyaona vipi? Kwa mujibu wa ile misimu minne inayopitiwa na binadamu, je, mtu yeyote anaweza kubadilisha sheria ya mabadilishano kati ya machipuko, kiangazi, mapukutiko na kipupwe? Wakati wa machipuko, miti huweza kuchomoza na kuchanua; katika kiangazi, inafunikwa na majani; katika mapukutiko inazaa matunda na katika kipupwe majani yanaanguka. Je, yupo anayeweza kubadilisha sheria hii? Je, hii inaonyesha dhana moja ya mamlaka ya Mungu? Mungu alisema “Iwe Nuru,” na ikawa nuru. Je, nuru hii ingali ipo? Nuru hii inakuwepo kwa ajili ya nini? Inakuwepo kwa sababu ya maneno ya Mungu, bila shaka, na kwa sababu ya mamlaka ya Mungu. Je, hewa iliyumbwa na Mungu bado ipo? Je, hewa ambayo binadamu anapumua inatoka kwa Mungu? Je, kuna yeyote anayeweza kuchukua vitu vinavyotoka kwa Mungu? Je, kuna yeyote anayeweza kubadilisha hali yao halisi na kazi? Kuna yeyote anayeweza kutibua mpangilio wa usiku na mchana kama ulivyopangwa na Mungu, na sheria ya usiku na mchana kama ilivyoamrisha na Mungu? Je, Shetani anaweza kufanya kitu kama hicho? Hata kama hulali wakati wa usiku, na unachukulia usiku kuwa wakati wa mchana, basi bado ni wakati wa usiku; unaweza kubadilisha mazoea yako ya kila siku, lakini huwezi kubadilisha sheria ya mabadilishano kati ya usiku na mchana—ukweli huu hauwezi

kubadilishwa na mtu yeyote, au sio? Kuna yeyote anayeweza kumfanya simba kulima ardhi kama afanyavyo ng’ombe? Je, yupo yeyote anayeweza kubadilisha ndovu kuwa punda? Je, yupo anayeweza kubadilisha kuku akapaa hewani kama tai? Je, yupo anayeweza kumfanya mbwa-mwitu kula nyasi kama kondoo? (La) Je, yupo anayeweza kumfanya samaki aliye majini kuishi kwenye ardhi kavu? Hilo haliwezi kufanywa na wanadamu. Na kwa nini haliwezi? Kwa sababu Mungu aliwaamuru samaki kuishi ndani ya maji, na kwa hivyo wanaishi ndani ya maji. Kwenye ardhi kavu hawataweza kuishi kwani watakufa; hawawezi kukiuka vipimo vya amri ya Mungu. Vitu vyote vina sheria na kipimo cha kuwepo kwao, na kila mojawapo kina silika zake binafsi. Haya yameamriwa na Muumba, na hayawezi kubadilishwa na kupitishwa na binadamu yeyote. Kwa mfano, simba siku zote ataishi jangwani, umbali fulani kutoka kwenye jumua ya binadamu, na hatawahi kuwa mtulivu na mwaminifu kama vile ng’ombe alivyo na anavyoishi na kumfanyia binadamu kazi. Ingawa ndovu na punda ni wanyama, na wote wana miguu minne, na ni viumbe vinavyopumua hewa, ni aina tofauti, kwani waligawanywa kwenye aina tofauti na Mungu, kila mmoja wao anazo silika zake binafsi, na hivyo hawatawahi kubadilishana. Ingawa kuku ana miguu miwili, na mbawa kama vile alivyo tai, hatawahi kuweza kupaa hewani; kama amejaribu sana anaweza tu kupaa hadi kwenye mti—na hili linaamuliwa na silika yake. Sina haja kusema, haya yote ni kwa sababu ya amri za mamlaka ya Mungu.

Katika maendeleo ya mwanadamu leo, sayansi ya mwanadamu inaweza kusemekana kwamba inanawiri, na mafanikio ya uchunguzi wa kisayansi wa binadamu unaweza kufafanuliwa kama wa kuvutia. Uwezo wa kibinadamu, lazima isemwe, unazidi kukua mkubwa zaidi, lakini kunao ushindi mmoja wa kisayansi ambao mwanadamu hajaweza kufanya: Mwanadamu ameunda ndege, vibebaji vya ndege, na hata bomu la atomiki, mwanadamu ameenda angani, ametembea mwezini, amevumbua Intaneti, na ameishi maisha ya kiwango cha juu ya teknolojia, ilhali mwanadamu hawezi kuumba kiumbe hai kinachopumua. Silika za kila kiumbe kilicho hai na sheria ambazo zinatawala kuishi kwake na mzunguko wa maisha na kifo wa kila kiumbe kilicho hai—vyote hivi haviwezekani na havidhibitiki na sayansi ya mwanadamu. Wakati huu, lazima isemekane kwamba haijalishi ni viwango gani vya juu zaidi vitakavyofikiwa na sayansi ya binadamu, haviwezi kulinganishwa na fikira zozote za Muumba na haiwezekani kutambua miujiza ya uumbaji wa Muumba na uwezo wa mamlaka Yake. Kunazo bahari nyingi sana juu ya nchi, ilhali hazijawahi kukiuka mipaka yao na kuja kwenye ardhi kwa nguvu, na hiyo ni kwa sababu Mungu aliwekea mipaka kila mojawapo ya bahari hizo; zilika popote pale Aliziamuru kukaa; na bila ya ruhusa ya Mungu haziwezi kusongasonga ovyo. Bila ya ruhusa ya Mungu, haziwezi kuingiliana, na zinaweza kusonga tu pale ambapo Mungu anasema hivyo, na pale ambapo zinaenda na kubakia ni suala na uamuzi wa mamlaka ya Mungu.

Ili kuweka wazi zaidi, “mamlaka ya Mungu” yanamaanisha kwamba ni wajibu wa Mungu.

Mungu anayo haki ya kuamua namna ya kufanya kitu na kinafanywa kwa vyovyote vile Anavyopenda. Sheria ya vitu vyote ni wajibu wa Mungu, na wala si wajibu wa binadamu; na wala haiwezi kubadilishwa na binadamu. Haiwezi kusongeshwa kwa mapenzi ya binadamu, lakini inaweza badala yake kubadilishwa kwa fikira za Mungu, na hekima ya Mungu, na amri za Mungu, na hii ni kweli ambayo haiwezi kukataliwa na binadamu yeyote. Mbingu na nchi na viumbe vyote, ulimwengu, mbingu yenye nyota, misimu minne ya mwaka, ile inayoonekana na isiyoonekana kwa binadamu—yote haya yapo, yanafanya kazi, na kubadilika bila ya kosa hata dogo, chini ya mamlaka ya Mungu, kulingana na shurutisho za Mungu, kulingana na amri za Mungu, na kulingana na sheria za mwanzo wa uumbaji. Si hata mtu mmoja au kifaa kimoja kinaweza kubadilisha sheria zao, au kubadilisha mkondo wa asili ambao sheria hizi zinafanya kazi; zilianza kutumika kwa sababu ya mamlaka ya Mungu, na zitaangamia kwa sababu ya mamlaka ya Mungu. Haya ndiyo mamlaka yenyewe ya Mungu. Sasa kwa sababu haya yote yamesemwa, je, unahisi kwamba mamlaka ya Mungu ni ishara ya utambulisho na ishara ya Mungu? Je, mamlaka ya Mungu yanaweza kumilikiwa na kiumbe chochote kilichoumbwa au ambacho hakijaumbwa? Yanaweza kuigwa, kufananishwa, au kubadilishwa na mtu yeyote, na kitu chochote, au kifaa chochote?

Utambulisho wa Muumba ni wa Kipekee, na Hufai Kufuata lile Wazo la Imani ya Kuabudu Miungu Wengi

Ingawa mbinu na uwezo wa Shetani ni kubwa zaidi kuliko zile za binadamu, Ingawa anaweza kufanya mambo ambayo hayawezi kufanywa na binadamu, bila kujali kama waonea wivu au unatamani kile ambacho Shetani anafanya, bila kujali kama unachukia au unachukizwa na kile anachofanya, bila kujali kama unaweza au huwezi kuona hicho, bila kujali ni kiwango kipi ambacho Shetani anaweza kutimiza au ni watu wangapi anaweza kudanganya ili wakamwabudu na kumtolea kafara, na bila kujali ni vipi unavyomfafanua, haiwezekani wewe kusema kwamba Shetani anayo mamlaka na nguvu za Mungu. Unafaa kujua kwamba Mungu ni Mungu, tunaye Mungu mmoja tu, na zaidi ya yote unafaa kujua kwamba ni Mungu tu aliye na mamlaka, na kwamba Anazo nguvu za kudhibiti na kutawala viumbe vyote. Eti kwa sababu Shetani anao uwezo wa kudanganya watu, na anaweza kujifanya kuwa Mungu, na anaweza kuiga ishara na miujiza inayofanywa na Mungu, amefanya mambo sawa na yale ya Mungu, wewe unasadiki kimakosa kwamba Mungu si wa kipekee, kwamba tunayo miungu mingi, kwamba tofauti yao ni kule kuwa tu na mbinu nyingi au chache zaidi, na kwamba kunazo tofauti katika upana na nguvu zinazoonyeshwa. Unapima ukubwa wao katika mpangilio wa kuwasili kwao, na kulingana na umri wao, na unasadiki kwa njia isiyofaa kwamba kunayo miungu mingine mbali na Mungu, na unafikiri kwamba nguvu na mamlaka ya Mungu si ya kipekee. Kama unazo fikira kama hizo, kama hutambui upekee wa Mungu, husadiki ni Mungu pekee

anayemiliki mamlaka na kama unatiiutatii tu imani ya kuabudu miungu wengi, basi Nasema kwamba wewe ni duni kabisa kuliko viumbe vyote, wewe ni mfano halisi na wa kweli wa Shetani, na wewe ni mtu kamili wa maovu! Je, unaelewa kile Ninachojaribu kufunza kwa kusema maneno haya? Haijalishi ni muda gani, mahali au maelezo ya ziada kuhusu wewe, haifai kuchanganya Mungu na mtu yeyote mwingine, kitu au kifaa. Haijalishi unavyohisi kwamba mamlaka ya Mungu na hali halisi ya Mungu Mwenyewe havijulikani wala kuweza kufikiwa, haijalishi ni kiwango kipi cha matendo na maneno ya Shetani yanavyokubaliana na mawazo na fikira zako, haijalishi ni vipi ambavyo mambo haya yanakutosheleza wewe, usiwe mjinga, usichanganye dhana hizi, usikatae uwepo wa Mungu, usikatae utambulisho na hadhi ya Mungu, usimsukume Mungu nje ya mlango na kumleta Shetani kuchukua nafasi ya “Mungu” aliye ndani ya moyo wako na kuwa Mungu wako. Sina shaka kwamba una uwezo wa kufikiria athari za kufanya hivyo!

Ingawa Binadamu Amepotoka, Angali Anaishi Chini ya Ukuu wa Mamlaka ya Muumba

Shetani amekuwa akipotosha mwanadamu kwa maelfu ya miaka. Ameleta kiwango kisichosemezeka cha maovu, amedanganya vizazi baada ya vizazi, na ametenda uhalifu wa kuchukiza ulimwenguni. Amedhulumu binadamu, amedanganya binadamu, ameshawishi binadamu ili ampinge Mungu, na ametenda vitendo vya maovu ambavyo vimetatiza na kuharibu mpango wa Mungu mara kwa mara. Ilhali, chini ya mamlaka ya Mungu, viumbe vyote na viumbe vyenye uhai vinaendelea kutii kanuni na sheria zilizowekwa wazi na Mungu. Yakilinganishwa na mamlaka ya Mungu, asili ovu ya Shetani na kuenea kwake ni vitu vibaya mno, vinakera mno na ni vya kuleta aibu na ni vidogo mno na vinyonge. Hata Ingawa Shetani anatembea miongoni mwa viumbe vyote vilivyoubwa na Mungu, hawezi kutekeleza mabadiliko madogo zaidi kwa watu, vitu, na vifaa vilivyoamriwa na Mungu. Miaka elfu kadhaa imepita, na mwanadamu angali anafurahia nuru na hewa aliyopewa na Mungu, angali anapumua pumzi iliyotolewa na Mungu Mwenyewe, angali anafurahia maua, ndege, samaki na wadudu walioubwa na Mungu, na kufurahia viumbe vyote vilivyotolewa na Mungu; mchana na usiku zingali zinabadilishana nafasi zao bila kusita; hiyo misimu minne inabadilishana kama kawaida; nao batabukini wanaopaa wanaondoka msimu huu wa kipupwe, lakini bado watarudi kwenye msimu ujao wa machipuko; samaki ndani ya maji hawajawahi kuondoka kwenye mito, maziwa—maskani yao; wadudu aina ya nyenje kwenye mchanga wanaimba kwelikweli kwenye siku za kiangazi; nyenje kwenye nyasi wanaimba kwa sauti ya polepole huku wakikaribisha msimu wa mapukutiko, wale batabukini wanaanza kutembea kwa makundi, huku nao tai wanabakia pweke; fahari za simba wakijitosheleza wenyewe kwa kuwinda; nao kunguni wa kaskazini wa Ulaya hawatoki kwenye nyasi na maua.... Kila aina ya kiumbe kilicho hai miongoni mwa viumbe vyote kinaondoka na kurudi, kisha kinaondoka tena, mabadiliko milioni

yanafanyika kwa muda wa kufumba na kufumbua—lakini kile kisichobadilika ni silika zao na sheria za kusalia. Wanaishi katika ruzuku na kustawishwa na Mungu, na hakuna mtu anayeweza kubadilisha silika zao, na vilevile hakuna mtu yeyote anayeweza kukiuka sheria hizi za kuishi. Ingawa mwanadamu, anayeishi miongoni mwa viumbe vyote amepotoka na kudanganywa na Shetani, angali hawezi kupuuza maji yaliyoubwa na Mungu, hewa iliyoubwa na Mungu, na vitu vyote vilivyoubwa na Mungu, na binadamu angali bado anaishi na kuzaana kwenye anga hii iliyoubwa na Mungu. Silika za mwanadamu zingali hazijabadilika. Binadamu angali anategemea macho yake kuona, masikio yake kusikia, ubongo wake kufikiria, moyo wake kuelewa, miguu na viganja vyake kutembea, mikono yake kufanya kazi, na kadhalika; silika zote ambazo Mungu alimpa binadamu ili aweze kukubali toleo la Mungu limebakia hivyo bila kubadilishwa, welekevu ambao binadamu alitumia kushirikiana na Mungu bado haujabadilika, welekevu wa mwanadamu wa kutenda wajibu wa kiumbe kilichoumbwa haujabadilishwa, mahitaji ya kiroho ya mwanadamu hayajabadilika, tamania la mwanadamu kuweza kujua asili zake halijabadilika, hamu ya mwanadamu kuweza kuokolewa na Muumba haijabadilika. Hizi ndizo hali za sasa za mwanadamu, anayeishi katika mamlaka ya Mungu, na ambaye amevumilia maangamizo mabaya yaliyoletwa na Shetani. Ingawa mwanadamu amepitia unyanyasaji wa Shetani, na yeye si Adamu na Hawa tena kutoka mwanzo wa uumbaji, badala yake amejaa mambo ambayo yana uadui na Mungu kama vile maarifa, fikira na kadhalika, na amejaa tabia ya kishetani iliyopotoka, kwenye macho ya Mungu, mwanadamu yungali bado mwanadamu yule yule Aliyemuumba. Mwanadamu angali anatawaliwa na kupangiwa na Mungu, na angali anaishi ndani ya mkondo uliowekwa wazi na Mungu, na kwa hivyo kwenye macho ya Mungu, mwanadamu ambaye amepotoshwa na Shetani amefunikwa tu na uchafu na tumbo linalonguruma, na miitikio ambayo ni ya kujikokota kidogo, kumbukumbu ambayo si nzuri kama ilivyokuwa, na ni mzee kidogo—lakini kazi na silika zote za binadamu bado hazijapata madhara kamwe. Huyu ndiye mwanadamu ambaye Mungu ananua kuokoa. Mwanadamu huyu anahitaji tu kusikia mwito wa Muumba na kusikia sauti ya Muumba, naye atasimama wima na kukimbia kutafuta ni wapi sauti imetokea. Mwanadamu huyu lazima tu aweze kuona umbo la Muumba naye hatakuwa msikivu wa kila kitu kingine, ataacha kila kitu, ili kuweza kujitolea mwenyewe kwa Mungu, na hata atayatenga maisha yake kwa ajili Yake. Wakati moyo wa mwanadamu unapoelewa maneno hayo ya moyoni kutoka kwa Muumba, mwanadamu atakataa Shetani na atakuja upande wake Muumba; wakati mwanadamu atakuwa ametakasa kabisa uchafu kutoka kwenye mwili wake, na amepokea kwa mara nyingine toleo na ukuzaji kutoka kwa Muumba, basi kumbukumbu la mwanadamu litarejeshwa, na kwa wakati huu mwanadamu atakuwa amerejea kwa kweli katika utawala wa Muumba.

Desemba 14, 2013

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee II

Tabia ya Haki ya Mungu

Kwa vile sasa mmesikiliza ushirika uliopita kuhusu mamlaka ya Mungu, Ninao ujasiri kwamba mmejihami vilivyo na mseto wa maneno kuhusu suala hili. Kiwango unachoweza kukubali, kufahamu, na kuelewa vyote hivi vinategemea na jitihada zipi utakazotumia. Ni tumaini Langu kwamba utaweza kutazamia suala hili kwa dhati; kwa vyovyote vile hufai kulishughulikia shingo upande! Sasa, je, kujua mamlaka ya Mungu ni sawa na kujua Mungu kwa uzima wake? Mtu anaweza kusema kwamba kujua mamlaka ya Mungu ndiyo mwanzo wa kumjua Mungu mwenyewe kwa upekee wake, na mtu anaweza kusema pia kwamba kuyajua mamlaka ya Mungu kunamaanisha kwamba mtu tayari ameingia kwenye lango kuu la kujua hali halisi ya ule upekee wa Mungu Mwenyewe. Ufahamu huu ni sehemu moja ya kumjua Mungu. Sehemu ile nyingine ni nini, hivyo basi? Hii ndiyo mada ambayo Ningependa tuweze kushiriki pamoja leo—tabia ya haki ya Mungu.

Nimeteua sehemu mbili kutoka kwenye Biblia ambazo ningependa tushiriki pamoja kuhusu mada ya leo: Jambo la kwanza linahusu kuangamizwa kwa Sodoma na Mungu, ambalo linaweza kupatikana kwenye Mwanzo 19:1-11 na Mwanzo 19:24-25; jambo la pili linahusu ukombozi wa Ninawi na Mungu, ambalo linaweza kupatikana kwenye kitabu cha Yona 1:1-2, kuongezea sura zile za tatu na nne za kitabu hiki. Ninashuku kwamba nyinyi nyote mnasubiri kusikia kile Nilicho nacho kuhusu sehemu hizi mbili. Kile Ninachosema hakiwezi kwenda kando na mada ya kutaka kumjua Mungu Mwenyewe na kujua hali Yake halisi, lakini ni nini kitakachokuwa zingatia la ushirika wa leo? Je, yupo yeyote kati yenu anayejua? Ni sehemu zipi za ushirika Wangu kuhusu “Mamlaka ya Mungu” ziliweza kuwavutia? Kwa nini Nilisema kwamba yule tu anayemiliki mamlaka na nguvu kama hizo ndiye Mungu mwenyewe? Ni nini Nilichotaka kuelezea kwa kusema hivyo? Ni nini ambacho Nilipenda kukufahamisha kuhusu? Je, mamlaka na nguvu za Mungu ni mtazamo mmoja unaoelezea kuhusu hadhi Yake halisi na inavyoonyeshwa? Je, mamlaka na nguvu hizi ni sehemu ya hali Yake halisi ambayo inathibitisha utambulisho Wake na hadhi? Je, maswali haya yamekufahamisha kile Ninachoenda kusema? Ni nini Ninachotaka uelewe? Fikiria hili kwa makini.

Kwa Kupinga Mungu kwa Ukaidi, Binadamu Anaangamizwa na Hasira za Mungu

Kwanza, hebu tuweze kuangalia mafungu mbalimbali ya maandiko yanayofafanua kuangamizwa kwa Sodoma na Mungu.

Mwa 19:1-11 Na jioni malaika wawili walikuja Sodoma; naye Lutu aliketi katika lango la

Sodoma: na baada ya Lutu kuwaona aliinuka kwenda kuwakaribisha; na akasujudu; Naye akasema, Tazama saa hii, bwana zangu, ingieni ndani, nawaomba, ndani ya nyumba ya mtumishi wenu, na mbaki usiku mzima, na msafishe miguu yenu, na mtaamka mapema, na mshike njia zenu. Nao wakasema, La; lakini tutaketi katika uwanja usiku mzima. Na akawaomba sana; na wakamjia na kuingia katika nyumba yake; na akawaandalia karamu, na kupika mikate bila chachu, na wakala. Lakini kabla ya wao kujilaza, watu kutoka mjini, hata wenyeji wa Sodoma, waliizunguka nyumba hiyo, wazee na pia vijana, watu wote kutoka kila sehemu: Na wakamwita Lutu, na kumwambia, Wako wapi wale wanaume waliokuja kwako leo usiku? Walete kwetu, ili tupate kuwajua. Naye Lutu akatoka mlangoni mahali walipokuwa, na akafunga mlango nyuma yake, Na kusema, nawaomba, ndugu, msitende maovu hivyo. Tazameni sasa, ninao mabinti wawili ambao ni mabikira; mniruhusu, nawaomba, niwalete nje kwenu, na mwafanyie mwonavyo kuwa vizuri katika macho yenu: ila kwa hawa wanaume msifanye chochote: kwani wamekuja chini ya kivuli cha paa langu. Na walisema. Toka. Na wakasema tena, Mtu huyu mmoja aliingia kwetu kukaa kwa muda, naye anatamani kuhukumu: sasa tutakushughulikia kwa njia mbaya zaidi, kuliko wao. Na wakamshinikiza sana mtu huyo, hadi Lutu, na wakawa karibu kuuvunja mlango. Lakini watu wale wakanyosha mbele mkono wao, na kumvuta Lutu katika nyumba walikokuwa, na kuufunga mlango. Na wakawagonga wale watu waliokuwa katika mlango wa nyumba na upofu, wakubwa na wadogo: kiasi kwamba walijichosha kuutafuta mlango.

Mwa 19:24-25 Kisha Yehova alinyesha kwa Sodoma na Gomora kibiriti na moto kutoka Yehova kutoka mbinguni; Na Akaiangusha hiyo miji, na mabonde yote, na wenyeji wote wa miji hiyo, na kile kilichomea kutoka ardhini.

Kutoka kwenye mafungu haya, si vigumu kuona kwamba dhambi ya Sodoma na kupotoka kwake tayari vilikuwa vimefikia kiwango kilichochukiza binadamu na Mungu, na kwamba kwa macho ya Mungu mji ulifaa kuangamizwa. Lakini nini kilichofanyikia mji huu hapo awali kabla haujaangamizwa? Ni msukumo upi tunaoweza kupata kutoka kwenye matukio haya? Je, mtazamo wa Mungu katika matukio haya unatuonyesha nini kuhusu tabia yake? Ili kuelewa hadithi nzima, hebu na tuweze kusoma kwa makini kile kilichorekodiwa katika Maandiko ...

Kupotoka kwa Sodoma: Kunakasirisha Binadamu, Kunaghadhibisha Mungu

Kwenye usiku huo, Lutu alipokea wajumbe wawili kutoka kwa Mungu na akawatayarishia karamu. Baada ya chajio, kabla hawajalala, watu kutoka kila pahali kwenye mji walizunguka makazi ya Lutu na kumwita nje Lutu. Maandiko yanawarekodi wakisema, “Wako wapi wale wanaume waliokuja kwako leo usiku? Walete kwetu, ili tupate kuwajua.” Ni nani aliyesema maneno haya? Alikuwa akiwaambia kina nani? Haya yalikuwa maneno ya watu wa Sodoma,

walipiga mayowe nje ya makazi ya Lutu wakinuia kumwita Lutu. Je, unahisi vipi ukiyasikia maneno haya? Unaghadhibishwa? Je, maneno haya yanakuhuzunisha? Je, unabubujikwa na hasira kali? Je, Huoni kwamba maneno haya yananuka Shetani? Kupitia kwa maneno haya, unaweza kuhisi uovu na giza vilivyomo kwenye mji huu? Je, unaweza kuhisi ukatili na ushamba wa tabia za watu hawa kupitia kwa maneno yao? Je, unaweza kuhisi kina cha kupotoka kwao kupitia kwa tabia yao? Kupitia kwa maudhui ya hotuba yao, si vigumu kuona kwamba asili yao ya dhambi na tabia yao iliyopotoka ilikuwa imefikia kiwango kilichokuwa zaidi ya wao kuidhibiti. Isipokuwa Lutu, kila mtu katika mji huu hakuwa tofauti na Shetani; ule mtazamo tu wa mtu mwingine uliwafanya watu hawa kutaka kudhuru na kuwapotosha wao.... Mambo haya hayampatii tu mtu hisia ya asili potovu na ya kutisha ya mji huu, lakini pia yanamwonyesha harufu ya kifo iliyozunguka mji huu; yanampa pia mtu hisia za dhambi na umwagikaji wa damu.

Alipojipata uso kwa uso na genge la majambazi waliojaa ukatili, watu waliokuwa wamejaa na maono ya kupotosha nafsi, Lutu aliitikia vipi? Kulingana na Maandiko: “Nawaomba ... msitende maovu hivyo. Tazameni sasa, ninao mabinti wawili ambao ni mabikira; mniruhusu, nawaomba, niwalete nje kwenu, na mwafanyie mwonavyo kuwa vizuri katika macho yenu: ila kwa hawa wanaume msifanye chochote: kwani wamekuja chini ya kivuli cha paa langu.” Lutu alimaanisha yafuatayo katika maneno yake: Alikuwa radhi kuwatoa binti zake wawili ili kuwalinda wale wajumbe. Kutokana na akili razini, watu hawa wangekubali masharti ya Lutu na kuwaacha wale wajumbe wawili pekee; kwani hata hivyo, wajumbe hao walikuwa watu wageni kabisa kwao, watu ambao hawakuwa na chochote katu kuhusiana na wao; wajumbe hawa wawili walikuwa hawajawahi kudhuru masilahi yao. Hata hivyo, wakiwa na motisha ya asili yao ya dhambi, hawakuliwachia suala hili hapo. Badala yake, walizidisha tu jitihada zao. Hapa mojawapo ya mabishano yao yanaweza bila shaka kumpatia mtu maono zaidi kuhusu asili ya kweli na potovu ya watu hawa; wakati uo huo yanatujaza na kutufanya tuelewe sababu ya Mungu kutaka kuuangamiza mji huu.

Kwa hivyo walisema nini baadaye? Kama vile Biblia inavyosoma: “Toka. Na wakasema tena, Mtu huyu mmoja aliingia kwetu kukaa kwa muda, naye anatamani kuhukumu: sasa tutakushughulikia kwa njia mbaya zaidi, kuliko wao. Na wakamshinikiza sana mtu huyo, hadi Lutu, na wakawa karibu kuuvunja mlango.” Kwa nini walitaka kuuvunja mlango? Sababu ni kwamba walikuwa na hamu ya kuwaletea madhura wale wajumbe wawili. Wale wajumbe walikuwa wakifanya nini Sodoma? Kusudio lao la kuja hapo lilikuwa ni kumwokoia Lutu na familia yake; hata hivyo, watu wa mji huo walifikiri kimakosa kwamba walikuwa wamekuja kuchukua nyadhifa zao rasmi. Bila ya kuulizia kusudio lao, ilikuwa tu hali ya kujiamulia kufanya mambo kabla ya kujua ukweli wake, iliyofanya mji huo kutaka kuwadhuru vibaya wajumbe

hawa wawili; walitaka kuwadhuru watu wawili ambao hawakuhusiana kwa vyovyote vile na wao. Ni wazi kwamba watu wa mji huu walikuwa wamepoteza kabisa ubinadamu na akili zao razini. Kiwango cha wendawazimu wao na kukosa ustaarabu kwao kilikuwa tayari si tofauti na asili potovu ya Shetani ya kudhuru na kudanganya binadamu.

Walipowaamuru watu hawa watoke kwa Lutu, Lutu alifanya nini? Kutoka kwenye maandishi yanayofuata tunajua kwamba Lutu hakuwakabidhi wajumbe hawa kwa watu hawa. Je, Lutu aliwajua wajumbe hawa wawili wa Mungu? Bila shaka la! Lakini kwa nini aliweza kuwaokoa watu hawa wawili? Je, alijua ni nini walichokuwa wamekuja kufanya? Ingawaje hakujua kuhusu sababu yao ya kuja, alijua kwamba walikuwa ni watumishi wa Mungu, na kwa hivyo aliwapokea. Kwamba aliweza kuwaita watumishi hawa wa Mungu mabwana yaonyesha kwamba Lutu kwa kawaida alikuwa ni mfuasi wa Mungu, tofauti na wale wengine waliokuwa ndani ya Sodoma. Kwa hivyo, wakati wajumbe wa Mungu walipomjia, alihatarisha maisha yake binafsi ili kuwapokea watumishi hao wawili; aidha, aliwatoa binti zake wawili kuwabadilisha na watumishi hao wawili ili kuwalinda watumishi hao. Hiki ndicho kilikuwa kitendo cha haki cha Lutu; vilevile lilikuwa onyesho linaloonekana waziwazi kuhusu asili na hali halisi ya Lutu, na ndiyo pia sababu ya Mungu kuwatuma watumishi Wake ili kumwokoza Lutu. Wakati alipokabiliwa na changamoto, Lutu aliwalinda watumishi hawa wawili bila kujali chochote kingine; alijaribu hata kufanya biashara ya kuwabadilisha binti zake wawili mradi tu watumishi hawa wapate usalama. Mbali na Lutu, kulikuwa na mtu yeyote mwingine ndani ya mji ambaye angefanya jambo kama hili? Kama vile hoja zinavyohibitisha—la! Kwa hivyo, ni wazi kabisa kwamba kila mtu katika Sodoma, isipokuwa Lutu, alikuwa mlengwa wa kuangamizwa pamoja na mlengwa aliyestahili kuangamizwa.

Sodoma Yaangamizwa kwa Kukosea Hasira za Mungu

Wakati watu wa Sodoma walipowaona watu hawa wawili, hawakuuliza sababu ya wao kuja wala hakuna yule aliyeuliza kama walikuwa wamekuja kueneza mapenzi ya Mungu. Kinyume cha mambo, walikusanyika na kuwa umati wa watu na, bila kusubiri ufafanuzi wowote, walikuja kuwakamata watumishi hawa wawili ni kana kwamba walikuwa mbwa koko au mbwa mwitu. Je, Mungu aliyatazama mambo haya wakati yalipokuwa yakifanyika? Mungu alikuwa akifikiria nini katika moyo Wake kuhusiana na tabia hii ya binadamu, aina ya jambo hili? Mungu aliamua kuangamiza mji huu; Asingesita wala kusubiri, wala Asingeendelea kuonyesha subira yake. Siku yake ilikuwa imetimia, na kwa hivyo Aliweza kuweka wazi kazi Aliyopenda kufanya. Hivyo basi, Mwanzo 19:24-25 inasema, “Kisha Yehova alinyesha kwa Sodoma na Gomora kibiriti na moto kutoka Yehova kutoka mbinguni; Na Akaiangusha hiyo miji, na mabonde yote, na wenyeji wote wa miji hiyo, na kile kilichomea kutoka ardhini.” Mistari hii miwili inawaambia watu

mbinu ambayo kwayo Mungu aliuangamiza mji huu; pia inawaambia watu kile ambacho Mungu aliangamiza. Kwanza, Biblia inasimulia kwamba Mungu aliunguza mji kwa moto, na kwamba kiwango cha moto kilikuwa tosha kuangamiza watu wote na kila kitu kilichomea kwenye ardhi. Hii ni kusema kwamba, moto ulioangushwa kutoka mbinguni haukuangamiza tu mji; uliangamiza pia watu wote na vitu vilivyo hai ndani yake, vyote bila kuacha chochote nyuma. Baada ya mji kuangamizwa, ardhi ilikuwa tupu bila kitu chochote kilicho hai. Hakukuwa tena na maisha, wala dalili zozote za maisha. Mji ulikuwa umebadilika na kuwa ardhi iliyoharibiwa, mahali patupu palipojaa kimya cha kutisha. Kusingekuwa na matendo maovu zaidi dhidi ya Mungu mahali hapa; kusingekuwa na uchinjaji zaidi au umwagikaji wa damu.

Kwa nini Mungu alitaka kuuchoma mji huu kabisa? Ni nini unachoweza kuona hapa? Je, Mungu angevumilia kumwona mwanadamu na asili, viumbe Vyake mwenyewe, vikiangamia hivi? Kama unaweza kutambua ghadhabu ya Yehova Mungu kutokana na moto ule ambao uliangushwa kutoka mbinguni, basi si vigumu sana kuona kiwango Chake cha hasira kali kutoka kwenye lengo la maangamizo Yake pamoja na kiwango ambacho mji huo uliweza kuangamizwa. Wakati Mungu anadharau mji, Ataweza kutekeleza adhabu Yake juu ya mji huo. Wakati Mungu anachukizwa na mji, Ataweza kutoa maonyo mbalimbali akifahamisha watu kuhusu ghadhabu Yake. Hata hivyo, wakati Mungu anaamua kukomesha na kuangamiza mji—yaani, wakati hasira na adhama Yake vimekosewa—Hataweza kutoa maonyo au adhabu nyingine. Badala yake, Ataweza kuuangamiza moja kwa moja. Ataufanya kutoweka kabisa. Hii ndiyo tabia ya haki ya Mungu.

Baada ya Ukinzani wa Mara kwa Mara wa Sodoma na Ukatili Wao Dhidi Yake, Mungu Anaufuta Kabisa

Mara tu tunapokuwa na ufahamu wa jumla kuhusu tabia ya haki ya Mungu, tunaweza kurejesha umakinifu wetu kwenye mji wa Sodoma—kile ambacho Mungu aliona kuwa mji wa dhambi. Kwa kuelewa hali halisi ya mji huu, tunaweza kuelewa ni kwa nini Mungu alitaka kuuangamiza na ni kwa nini Aliuangamiza kabisa. Kutokana na haya, tunaweza kujua tabia ya haki ya Mungu.

Kutoka katika mtazamo wa binadamu, Sodoma ulikuwa ni mji ulioweza kutosheleza kikamilifu matamanio ya binadamu na maovu ya binadamu. Ulivutia na uliduwaza, kwa muziki na densi usiku baada ya usiku, ufanisi wake uliwasukuma wanaume kufurahia na kuruka kichwa. Maovu yake yalidhuru mioyo ya watu na yakawaduwaza hadi kuzoroteka. Huu ulikuwa mji uliokuwa na roho chafu na roho za Shetani zilicharuka hewani; ulijaa dhambi na mauaji na harufu ya damu iliyovunda. Ulikuwa mji ambao ulitisha watu kabisa, mji ambao mtu angejitoa kwake kwa hofu. Hakuna mtu katika mji huu—awe wa kiume au wa kike, awe mchanga au

mzee—aliyetafuta njia ya kweli; hakuna aliyetamani mwangaza au kutaka kuachana na dhambi. Kila mmoja aliishi chini ya udhibiti wa Shetani, upotovu na uwongo. Kila mmoja alikuwa ameupoteza ubinadamu wake; walikuwa wamepoteza hisia zao, na walikuwa wamepoteza shabaha asilia ya kuweko kwa binadamu. Walitenda matendo maovu yasiyohesabika za ukinzani dhidi ya Mungu; walikataa mwongozo wake na kupinga mapenzi Yake. Yalikuwa matendo yao maovu ambayo yaliwapeleka watu hawa, mji na kila kiumbe kilichokuwa ndani ya mji huu, hatua kwa hatua, kwenye njia ya maangamizo.

Ingawaje mafungu haya mawili hayarekodi maelezo yanayofafanua kiwango cha kupotoka cha watu wa Sodoma, badala yake yanarekodi mwenendo wao kwa watumishi wawili wa Mungu kufuatia kuwasili kwao mjini, ukweli mtupu unaweza kufichua kiwango ambacho watu wa Sodoma walikuwa wamepotoka, walijaa maovu na walimpinga Mungu. Kwa mujibu wa haya, ukweli wa mambo na hali halisi ya watu wa mji huu vinafichuliwa pia. Mbali na kutokubali maonyo ya Mungu, hawakuogopa pia adhabu Yake. Kinyume cha mambo ni kwamba, walifanyia mzaha ghadhabu ya Mungu. Walimpinga Mungu bila sababu. Haijalishi ni nini Alichofanya au ni vipi Alivyokifanya, asili yao ya tamaa ilizidi kuongezeka, na wakampinga Mungu mara kwa mara. Watu wa Sodoma walikuwa wakatili kwa uwepo wa Mungu, kuja Kwake, adhabu Yake, na hata zaidi, maonyo Yake. Hawakuona chochote kingine chenye thamani karibu nao. Waliwapotosha na kuwadhuru watu wote walioweza kupotoshwa na kupata madhara, na wakawatendea watumishi wa Mungu vivyo hivyo. Kuhusiana na matendo yote ya uovu yaliyotendwa na watu hawa wa Sodoma, kuwadhuru watumishi wa Mungu kulikuwa mfano tu wa tone baharini ya kile walichokuwa wakifanya, na asili yao ya uovu uliofichuliwa kwa kweli ulionekana tu kuwa mdogo zaidi kuliko hata tone moja ndani ya bahari kubwa. Kwa hivyo, Mungu alichagua kuwaangamiza kwa moto. Mungu hakutumia gharika, wala Hakutumia zilizala, mtetemeko wa ardhi, sunami au mbinu yoyote nyingine ya kuuangamiza mji huu. Kule kutumia moto na Mungu kuangamiza mji huu kulimaanisha nini? Kulimaanisha uangamizaji kamili wa mji huo; kulimaanisha kwamba mji huu ulitoweka kabisa kutoka ulimwenguni na kutoka katika kuwepo kwake. Hapa, “kuangamiza” hakurejelei tu kule kutoweka kwa umbo na muundo au sura ya nje ya mji huo; kunamaanisha pia kwamba nafsi za watu ndani ya mji huo zilisita kuwepo, baada ya kufutwa kabisa. Kwa ufupi, watu wote, matukio na mambo yote yaliyohusiana na mji huu yaliangamizwa. Kusingekuwa na maisha ya baadaye au roho kuwa mwilini mwao tena; Mungu alikuwa amewafuta kabisa kutoka katika binadamu, uumbaji Wake, mara moja na tena milele. Yale “matumizi ya moto” yalimaanisha kusitisha dhambi, na yalimaanisha mwisho wa dhambi; dhambi hii ingesita kuwepo na kuenea. Yalimaanisha kwamba uovu wa Shetani ulikuwa umepoteza mahali pake pa kunawiri pamoja na eneo la kaburi ambalo liliupatia mji huo mahali pa kukaa na kuishi. Kwenye vita kati ya Mungu na Shetani, matumizi

ya moto na Mungu ni alama ya ushindi Wake ambayo Shetani anatajiwa. Kuangamizwa kwa Sodoma ni hatua kubwa ya kuzuia maono ya Shetani ya kupinga Mungu kwa kupotosha na kudanganya binadamu, na vilevile ni ishara ya kudhalilishwa kwa muda kwenye maendeleo ya binadamu ambapo binadamu alikataa mwongozo wa Mungu na akajiachilia kutenda maovu. Aidha, ni rekodi ya ufunuo wa kweli wa tabia ya haki ya Mungu.

Wakati ule moto ambao Mungu alituma kutoka mbinguni ulikuwa umeteketeza kabisa Sodoma hata zaidi ya majivu, ilimaanisha kwamba mji huu ulioitwa “Sodoma” ungesita kuwepo, na vilevile kila kitu ndani ya mji wenyewe. Uliangamizwa kwa ghadhabu ya Mungu; ulitoweka kutokana na hasira na adhama ya Mungu. Kwa sababu ya tabia ya haki ya Mungu Sodoma ilipokea adhabu yake ya haki; kutokana na tabia ya haki ya Mungu, ilipokea mwisho wake wa haki. Mwisho wa kuwepo kwa Sodoma ulitokana na maovu yake, na ulitokana pia na tamanio la Mungu kutowahi kuutazamia mji huu tena, pamoja na watu wote walioishi ndani ya mji huo au maisha yoyote yaliyowahi kukua ndani ya mji huo. “Tamanio la kutowahi kuutazamia mji huo tena” la Mungu ni hasira Yake, pamoja na adhama Yake. Mungu aliuteketeza mji kwa sababu maovu na dhambi zake vilimsababisha Yeye kuhisi ghadhabu, maudhi na chuki katika mji huu na tamanio lake la kutowahi kuuona au watu wowote wa mji huo na viumbe vyote vilivyo hai vilivyokuwa ndani ya mji huo tena. Baada ya mji huo kuacha kuchomeka, huku ukiwa umeacha nyuma jivu pekee, ulikuwa kwa kweli umesita kuwepo mbele ya macho ya Mungu; hata kumbukumbu za Mungu kuuhusu ziliondolewa, zilifutwa. Hii inamaanisha kwamba moto ulioangushwa kutoka mbinguni haukuangamiza tu mji wote wa Sodoma kwa jumla na watu waliokuwa wamejaa dhambi ndani yake, wala kuangamiza tu vitu vyote vilivyokuwa ndani ya mji uliokuwa umepatwa na dosari ya dhambi; hata zaidi, moto huu ulianguka kumbukumbu za maovu na ukinzani wa binadamu dhidi ya Mungu. Hili ndilo lilikuwa kusudio la Mungu kwa kuuchoma ule mji.

Binadamu ulikuwa umepotoka kupindukia. Watu hawa hawakujua Mungu alikuwa nani au kule walikokuwa wametokea. Kama ungemtaja Mungu, watu hawa wangekushambulia, kukutukana na kukufuru. Hata wakati watumishi wa Mungu walikuwa wamekuja kueneza onyo Lake, watu hawa waliopotoka hawakuweza kuonyesha ishara zozote za toba na hawakuacha mwenendo wao wa maovu, lakini kinyume cha mambo ni kwamba, waliweza bila ya haya, kuwadhuru watumishi wa Mungu. Kile walichoonyesha na kufichua kilikuwa asili na hali yao halisi ya uadui mkubwa kwa Mungu. Tunaweza kuona kwamba ukinzani wa watu hawa waliopotoka dhidi ya Mungu ulikuwa zaidi ya ufunuo wa tabia yao potovu, kama vile tu ilivyokuwa zaidi ya tukio la matusi au kejeli iliyotokana na ukosefu wa ufahamu wa ukweli. Ujinga wala kutojua havikusababisha mwenendo huu wa maovu; haikuwa kwa sababu watu hawa walikuwa wamedanganywa, na bila shaka si kwa sababu walikuwa wamepotoshwa.

Mwenendo wao ulikuwa umefikia kiwango cha uhasama wa wazi wa kupinga na kuasi dhidi ya Mungu. Bila shaka, aina hii ya tabia ya binadamu ingempa hasira kali Mungu, na ingesababisha hasira kali kwenye tabia Yake—tabia ambayo haitakiwi kukosewa. Kwa hivyo, Mungu aliachilia kwa njia ya moja kwa moja na kwa uwazi hasira Yake na adhama Yake; huu ni ufunuo wa kweli wa tabia Yake ya haki. Akiwa amekabiliwa na mji uliotiririka na dhambi, Mungu alitamani kuuangamiza kwa njia ya haraka zaidi iliyowezekana; Alipenda kuwaondoa watu waliokuwa ndani yake na uzima wa dhambi zao kwa njia kamilifu zaidi, kuwafanya watu hawa wa mji kusita kuwepo na kukomesha dhambi ndani ya mahali hapa kuongezeka. Njia ya haraka zaidi na kamilifu zaidi ya kufanya hivyo ilikuwa ni kuuteketeza kwa moto. Mtazamo wa Mungu kwa watu wa Sodoma haukuwa ule wa kuwaacha au kutowajali; bali, Alitumia hasira Yake, adhama na mamlaka kuwaadhibu, kuwaweka chini na kuwaangamiza kabisa watu hawa. Mtazamo wake kwao haukuwa tu ule wa kuwaangamiza kimwili bali pia kuwaangamiza kinafsi, ukomeshaji wa milele. Hii ndiyo athari ya kweli ya tamanio la Mungu kwao “kuweza kusita kuwepo.”

Ingawaje Hasira ya Mungu ni Fiche na Haijulikani kwa Binadamu, Haivumilii Kosa Lolote

Namna Mungu alivyoshughulikia binadamu wote wa ujinga na kutojua ulitokana kimsingi na huruma na uvumilivu. Hasira yake, kwa upande mwingine, imefichwa kwenye wingi mkubwa mno wa muda na wa mambo; haijulikani kwa binadamu. Kutokana na hayo, ni vigumu sana kwa binadamu kumwona Mungu akionyesha hasira Yake, na ni vigumu pia kuelewa hasira Yake. Kwa hivyo, binadamu huchukulia hasira ya Mungu kuwa ndogo. Wakati binadamu anakabiliwa na kazi ya mwisho ya Mungu na hatua ya kuvumilia na kusamehe binadamu—yaani, wakati onyesho la mwisho la Mungu la huruma na onyo Lake la mwisho linapowafikia—kama bado wangali wanatumia mbinu zile kumpinga Mungu na hawafanyi jitihada zozote za kutubu, kurekebisha njia zao au kukubali huruma Yake, Mungu hataweza tena kuwapatia uvumilivu na subira yake. Kinyume cha mambo ni kwamba, ni katika wakati huu ambapo Mungu atafuta huruma Yake. Kufuatia hili, Atatuma tu hasira Yake. Anaweza kuonyesha hasira Yake kwa njia tofauti, kama vile tu Anavyoweza kutumia mbinu tofauti kuwaadhibu na kuwaangamiza watu.

Matumizi ya Mungu ya moto kuuangamiza mji wa Sodoma ndio mbinu Yake ya haraka zaidi ya kuondoa kabisa binadamu au kitu. Kuwachoma watu wa Sodoma kuliangamiza zaidi ya miili yao ya kimwili; kuliangamiza uzima wa roho zao, nafsi zao na miili yao, na kuhakikisha kwamba watu waliokuwa ndani ya mji wangesita kuwepo kwenye ulimwengu wa anasa na hata ulimwengu usioonekana na mwanadamu. Hii ni njia moja ambayo Mungu hufichua na kuonyesha hasira Yake. Mfano huu wa ufunuo na maonyesho ni dhana moja ya hali halisi ya hasira ya Mungu, kama vile ilivyo kwa kawaida pia ufunuo wa hali halisi ya tabia ya haki ya Mungu. Wakati Mungu anaposhusha hasira Yake, Yeye husita kufichua huruma au upole wa

upendo wowote, na wala haonyeshi tena uvumilivu au subira Yake; hakuna mtu, kitu au sababu inayoweza kumshawishi kuendelea kuwa na subira, kutoa huruma Yake tena, na kumpa binadamu uvumilivu wake kwa mara nyingine. Badala ya mambo haya, bila kusita hata kwa muda mfupi, Mungu atashusha hasira Yake na adhama, kufanya kile Anachotamani, na Atafanya mambo haya kwa haraka na kwa njia safi kulingana na matamania Yake binafsi. Hii ndiyo njia ambayo Mungu hushusha hasira na adhama Yake, ambavyo binadamu hatakiwi kukosea, na pia ni maonyesho ya dhana moja ya tabia Yake ya haki. Wakati watu wanashuhudia Mungu akionyesha wasiwasi na upendo kwa binadamu, hawawezi kugundua hasira Yake, kuiona uadhama Yake au kuhisi kutovumilia Kwake kosa. Mambo haya siku zote yamewaongoza watu kusadiki kwamba tabia ya haki ya Mungu ni ile ya huruma, uvumilivu na upendo tu. Hata hivyo, wakati mtu anapona Mungu akiuangamiza mji au akichukia binadamu, hasira Yake katika kuangamiza binadamu na adhama Yake huruhusu watu kuona kidogo upande ule mwingine wa tabia Yake ya haki. Huku ni kutovumilia kosa kwa Mungu. Tabia ya Mungu isiyovumilia kosa inavuka mawazo ya kiumbe chochote kilichoumbwa, na miongoni mwa viumbe ambavyo havikuumbwa, hakuna kati ya hivyo kinachoweza kuhitilafiana na kingine au kuathiri kingine; lakini hata zaidi, hakiwezi kughushiwa au kuigwa. Kwa hivyo, dhana hii ya tabia ya Mungu ndiyo ambayo binadamu anafaa kujua zaidi. Mungu Mwenyewe Pekee ndiye aliye na aina hii ya tabia, na Mungu Mwenyewe pekee ndiye anayemiliki aina hii ya tabia. Mungu anamiliki aina hii ya tabia kwa sababu Anachukia maovu, giza, maasi na vitendo vya uovu vya Shetani—vya kutosha na kudanganya wanadamu—kwa sababu Anachukia vitendo vyote vya dhambi vinavyompinga Yeye na kwa sababu ya hali Yake halisi takatifu na isiyo na doa. Ni kwa sababu ya haya ndiposa Hataacha viumbe vyovyote kati ya vile vilivyoundwa au ambavyo havikuumbwa vimpinge waziwazi au kushindana na Yeye. Hata mtu binafsi ambaye Aliwahi kumwonyesha huruma au kuchagua anahitaji tu kuchochea tabia Yake na kukiuka kanuni Yake ya subira na uvumilivu, na Ataachilia na kufichua tabia Yake ya haki bila ya huruma hata kidogo au kusitasita kokote—tabia isiyovumilia kosa lolote.

Hasira ya Mungu Ni Usalama wa Nguvu Zote za Haki na Mambo Yote Mazuri

Kwa kuielewa mifano hii ya unenaji wa Mungu, fikira na vitendo vya Mungu, je, unaweza kuielewa tabia ya haki ya Mungu, tabia isiyoweza kukosewa? Mwishowe, hii ni dhana ya tabia ya kipekee kwa Mungu Mwenyewe, bila ya kujali ni kiwango kipi ambacho binadamu anaweza kuelewa. Mungu kutoweza kuvumilia kosa ndicho kiini Chake cha kipekee; hasira ya Mungu ndiyo tabia Yake ya kipekee; adhama ya Mungu ndiyo hali Yake halisi ya kipekee. Kanuni inayoelezea ghadhabu ya Mungu inaonyesha utambulisho na hadhi ambayo Yeye tu ndiye anayemiliki. Mtu hana haja kutaja kwamba ni ishara pia ya hali halisi ya Mungu Mwenyewe wa kipekee. Tabia ya Mungu ndiyo hali Yake halisi ya asili. Haibadiliki kamwe na kupita kwa

muda, wala haibadiliki kila wakati mahali panapobadilika. Tabia Yake ya asili ndiyo kiini Chake halisi cha kweli. Haijalishi ni nani anayetokelezea kazi Yake, hali Yake halisi haibadiliki, na wala tabia ya haki Yake pia. Wakati mtu anapomghadhibisha Mungu, kile Anachomshushia ni tabia Yake ya asili; wakati huu kanuni inayoelezea ghadhabu Yake haibadiliki, wala utambulisho na hadhi Yake ya kipekee. Haghadhibishwi kwa sababu ya mabadiliko katika hali Yake halisi au kwa sababu ya tabia Yake kusababisha dalili tofauti, lakini kwa sababu upinzani wa binadamu dhidi Yake huikosea tabia Yake. Uchochezi waziwazi wa binadamu kwa Mungu ni changamoto kubwa katika utambulisho na hadhi binafsi ya Mungu. Kwa mtazamo wa Mungu, wakati binadamu anapompinga Yeye, binadamu huyo anashindana na Yeye na anampima ghadhabu Yake. Wakati binadamu anapompinga Mungu, wakati binadamu anashindana na Mungu, wakati binadamu anapojaribu kila mara ghadhabu ya Mungu—na ndio maana pia dhambi huongezeka—hasira ya Mungu itaweza kufichuka kwa kawaida na kujitokeza yenyewe. Kwa hivyo, maonyesho ya Mungu ya hasira Yake yanaashiria kwamba nguvu zote za maovu zitasita kuwepo; yanaashiria kwamba nguvu zote katili zitaangamizwa. Huu ndio upekee wa tabia ya haki ya Mungu, na ndio upekee wa hasira ya Mungu. Wakati heshima na utakatifu wa Mungu vinapopata changamoto, wakati nguvu za haki zinapata kuzuiliwa na hazionekani na binadamu, Mungu atashusha hasira Yake. Kwa sababu ya hali halisi ya Mungu, nguvu hizo zote ulimwenguni zinazoshindana na Mungu, zinazompinga Yeye na kushindana na Yeye ni za maovu, kupotoka na kutokuwa na dhalimu; zinatoka Kwake na zinamilikiwa na Shetani. Kwa sababu Mungu ni wa haki, wa nuru na mtakatifu bila dosari, vitu vyote viovu, vilivyopotoka na vinavyomilikiwa na Shetani vitatoweka baada ya kuachiliwa kwa hasira ya Mungu.

Ingawaje kumwagwa kwa hasira ya Mungu ni dhana ya maonyesho ya tabia ya haki Yake, hasira ya Mungu kwa vyovyote vile haibagui walengwa wake au haina kanuni. Kinyume cha mambo ni kwamba, Mungu si mwepesi wa ghadhabu, wala Hakimbili kufichua hasira Yake na adhama Yake. Aidha, hasira ya Mungu inadhibitiwa na kupimwa kwa kiwango fulani; hailinganishwi kamwe na namna ambavyo binadamu atakavyowaka kwa hasira kali au kutoa ghadhabu zake. Mazungumzo mengi kati ya binadamu na Mungu yamerekodiwa kwenye Biblia. Maneno ya baadhi ya watu hawa binafsi yalikuwa ya juujuu, yasiyo na ujuzi na yasiyofaa, lakini Mungu hakuwaangusha chini, wala Hakuwashutumu. Hususan, wakati wa majaribio ya Ayubu, je, Yehova Mungu aliwachukuliaje marafiki watatu wa Ayubu na wale wengine baada ya kusikia maneno waliyomzungumzia Ayubu? Je, Aliwashutumu? Je, Aligeuka na kushikwa na hasira kali kwao? Hakufanya kitu kama hicho! Badala yake Alimwambia Ayubu kuwasihi, kuwaombea; Mungu, kwa mkono mwingine, hakuchukua lawama zao na kutia moyoni. Matukio haya yote yanawakilisha mtazamo mkuu ambao Mungu anashughulikia binadamu waliopotoka, na wasiojua. Kwa hivyo, kushushwa kwa hasira ya Mungu si kwa vyovyote vile maonyesho au hali

ya kutoa nje hali Yake ya moyo. Hasira ya Mungu si mlipuko mkubwa wa hasira kali kama vile binadamu anavyoielewa. Mungu hawachilii hasira Yake kwa sababu hawezi kuidhibiti hali ya moyo Wake binafsi au kwa sababu ghadhabu Yake imefikia kilele na lazima itolewe. Kinyume cha mambo ni kwamba, hasira Yake ni maonyesho ya tabia ya haki Yake na maonyesho halisi ya tabia ya haki Yake; ni ufunuo wa ishara ya hali Yake halisi takatifu. Mungu ni hasira, asiyeumilia kosa—hivi si kusema kwamba ghadhabu ya Mungu haitofautishi sababu za kufanya hivyo au haifuati kanuni; ni binadamu uliopotoka ambao unafuata mkondo wa kipekee wa kutokuwa na kanuni, mlipuko wa hasira kali bila mpango usiotofautisha hali hii miongoni mwa sababu mbalimbali. Mara tu binadamu anapokuwa na hadhi, mara nyingi atapata ugumu wa kudhibiti hali ya moyo wake, na kwa hivyo atafurahia kutumia nafasi mbalimbali kueleza kutotosheka kwake na kutoa nje hisia zake; mara nyingi atawaka kwa hasira kali bila sababu yoyote, ili kuonyesha uwezo wake na kuwafanya wengine kujua kwamba hadhi yake na utambulisho wake ni tofauti na ule wa watu wa kawaida. Bila shaka, watu waliopotoka wasiokuwa na hadhi yoyote mara kwa mara pia watapoteza udhibiti wao. Ghadhabu yao mara nyingi husababishwa na uharibifu wa manufaa yao ya kibinafsi. Ili kulinda hadhi yake binafsi na heshima, mwanadamu aliyepotoka mara kwa mara atatoa nje hisia zake na kufichua asili yake yenye kiburi. Binadamu atalipuka kwa ghadhabu na kutoa nje hisia zake ili kutetea na kushikilia uwepo wa dhambi, na matendo haya ndiyo njia ambayo kwayo binadamu anaonyesha kutotosheka kwake; yamejaa dosari, mifumo na mbinu mbalimbali, kupotoka na maovu ya binadamu, na zaidi ya chochote kingine, yanajaa kwa malengo na matamanio ya binadamu. Wakati haki inaposhindana na maovu, binadamu hataruka juu kwa ghadhabu ili kutetea uwepo wa haki; kinyume ni kwamba, wakati nguvu za haki zinatishwa, zinaonesha na kushambuliwa, mtazamo wa binadamu ni ule wa kutotilia maanani, kukwepa, au kushtuka. Hata hivyo, wakati anapokabiliwa na nguvu za maovu, mtazamo wa binadamu ni ule wa kutunza, na kunyenyekea mno. Hivyo basi, kutoa nje ghadhabu kwa binadamu ni kimbilio la nguvu za maovu, maonyesho ya mwenendo wa maovu uliokithiri na usiositishwa wa binadamu wa kimwili. Wakati Mungu anaposhusha hasira Yake, hata hivyo, nguvu zote za maovu zitasitishwa; dhambi zote za kudhuru binadamu zitasitishwa; nguvu zote katili zinazozuia kazi ya Mungu zitawekwa wazi, zitatenganishwa na kulaaniwa; washirika wote wa Shetani ambao wanampinga Mungu wataadhibiwa, na kuondolewa. Badala yake, kazi ya Mungu itaendelea huru bila vizuizi vyovyote; mpango wa usimamizi wa Mungu utaendelea kuimarika hatua kwa hatua kulingana na utaratibu uliopo; watu walioteuliwa na Mungu watakuwa huru dhidi ya kusumbuliwa na Shetani na kudanganywa; wale wanaomfuata Mungu watafurahia uongozi na ujazo wa Mungu miongoni mwa mazingira yenye utulivu na amani. Hasira ya Mungu ni usalama unaozuia nguvu zote za maovu dhidi ya kuzidishwa na kutapakaa kwa nguvu, na pia ni usalama unaolinda kuwepo na kuenea kwa mambo yote ya haki na mazuri na daima dawamu unayalinda mambo haya dhidi ya

kukandamizwa na kuangamizwa.

Unaweza kuona hali halisi ya hasira ya Mungu katika kuangamiza Kwake kwa Sodoma? Je, kuna jambo lolote lililochanganyika kwenye hasira Yake kali? Je, hasira kali ya Mungu ni safi? Ili kutumia maneno ya binadamu, je, hasira kali ya Mungu imetiwa najisi? Je, kunayo hila yoyote katika hasira Yake? Je, kunayo njama yoyote? Je, zipo siri zozote zisizotamkika? Ninaweza kukwambia wazi na kwa makini: Hakuna sehemu ya hasira ya Mungu inayoweza kumwongoza mtu kwa shaka. Ghadhabu yake haina kasoro, ni hasira ambayo haijatiwa najisi na haijasheheni nia au shabaha zozote zingine. Sababu ya ghadhabu Yake ni safi, haina lawama na haipingiki. Ni ufunuo wa kawaida na onyesho la hali Yake halisi ya utakatifu; ni kitu ambacho hakuna kiumbe chochote kinamiliki. Hii ni sehemu ya tabia ya kipekee ya haki ya Mungu, na ni tofauti ya wazi kati ya hali halisi husika ya Muumba na uumbaji Wake.

Haijalishi kama mtu anakuwa na ghadhabu akiwa mbele ya wengine au wakiwa hawako naye, kila mtu anayo nia na kusudi tofauti. Pengine wanajenga heshima zao, au pengine wanatetea masilahi yao binafsi, na kuendeleza taswira yao au kulinda sura yao. Baadhi yao huendeleza hali ya kuzuia ghadhabu yao, huku nao wengine wanakimbilia na wanapandwa na hasira kali kila wanapopenda bila ya hata kiwango kidogo zaidi cha kujizuia. Kwa ufupi, ghadhabu ya binadamu inatokana na tabia yake iliyopotoka. Haijalishi kusudi lake, ni la mwili na ni la asili; halina uhusiano wowote na haki au ukiukaji wa haki kwa sababu hakuna kitu katika asili ya binadamu na hali halisi vinavyolingana na ukweli. Kwa hivyo, hasira ya binadamu wapotovu na hasira ya Mungu vyote havifai kutajwa kwa kiwango sawa. Bila ubaguzi, tabia ya mwanadamu aliyepotoshwa na Shetani huanza na tamania la kulinda upotovu, na ina msingi katika upotovu; hivyo basi, hasira ya mwanadamu haiwezi kutajwa kwa kiwango sawa na ghadhabu ya Mungu, haijalishi ni bora namna gani kinadharia. Wakati Mungu anaposhusha hasira Yake kali, nguvu za giza zinakaguliwa, mambo ya giza yanaangamizwa, huku mambo ya haki na mazuri yakifurahia utunzaji wa Mungu, ulinzi, na yote yanaruhusiwa kuendelea. Mungu hushusha hasira Yake kwa sababu ya mambo dhalimu, mabaya na ya giza, yanayozuia, yanayotatiza au kuangamiza shughuli na maendeleo ya kawaida ya mambo ya haki na mazuri. Shabaha ya ghadhabu ya Mungu si kusalimisha hadhi na utambulisho Wake binafsi, lakini kusalimisha uwepo wa mambo ya haki, mazuri, ya kupendeza na kuvutia, kusalimisha sheria na mpangilio wa kuwepo kwa kawaida kwa binadamu. Hiki ndicho chanzo asilia cha hasira ya Mungu. Hasira kali ya Mungu ni bora sana, ya kiasili na ufunuo wa kweli wa tabia Yake. Hakuna makusudi yoyote katika hasira Yake kali, wala hakuna udanganyifu au njama yoyote; au hata zaidi, hasira Yake kali haina tamania lolote, ujanja, mambo ya kijicho, udhalimu, maovu, au kitu kingine ambacho binadamu wote waliopotoka huwa navyo. Kabla ya Mungu kushusha hasira Yake kali, huwa tayari Ametambua hali halisi ya kila suala kwa uwazi na ukamilifu zaidi,

na huwa tayari Amepangilia ufafanuzi na hitimisho sahihi na zilizo wazi. Hivyo basi, lengo la Mungu katika kila suala Analofanya ni wazi kabisa, vile ulivyo mtazamo Wake. Yeye si mtu aliyechanganyikiwa; Yeye si kipofu; Yeye si mtu wa kuamua ghafla; Yeye si mzembe; na zaidi, Yeye si mtu asiyefuata kanuni. Hii ndiyo dhana ya kimatendo ya hasira ya Mungu, na ni kwa sababu ya dhana hii ya kimatendo ya hasira ya Mungu ambapo binadamu umefikia uwepo wake wa kawaida. Bila ya hasira ya Mungu, binadamu ungeishia kuishi katika mazingira yasiyo ya kawaida; viumbe vyote vyenye haki, virembo na vizuri vingeamizwa na kusita kuwepo. Bila ya hasira ya Mungu, sheria na amri za kuwepo kwa viumbe vingekiukwa au hata kupinduliwa kabisa. Tangu uumbwaji wa binadamu, Mungu ametumia bila kusita, tabia Yake ya haki kusalimisha na kuendeleza uwepo wa kawaida wa binadamu. Kwa sababu tabia Yake ya haki inayo hasira na adhama, watu wote waovu, vitu, vifaa na vitu vyote vinavyotatiza na kuharibu uwepo wa kawaida wa binadamu vinaadhibiwa, vinadhibitiwa na kuangamizwa kwa sababu ya hasira Yake. Kwenye milenia mbalimbali zilizopita, Mungu ameendelea kutumia tabia Yake ya haki kuangusha na kuangamiza kila aina za roho chafu na za giza ambazo zinampinga Mungu na kuchukua nafasi ya wasaidizi na watumishi wa Shetani katika kazi ya Mungu ya kusimamia binadamu. Hivyo basi, kazi ya Mungu ya wokovu wa binadamu siku zote imeimarika kulingana na mpango Wake. Hivi ni kusema kwamba kwa sababu ya uwepo wa hasira ya Mungu, sababu za haki zaidi za binadamu hazijawahi kuangamizwa.

Sasa kwa vile unao ufahamu wa hali halisi ya hasira ya Mungu, bila shaka lazima utakuwa na ufahamu bora zaidi wa namna ya kutofautisha maovu ya Shetani!

Ingawa Shetani Anaonekana Mwenye Utu, Haki na Maadili, Ni Mkatili na Mwovu katika Kiini Chake

Shetani hupata umaarufu wake kupitia kwa kuudanganya umma. Mara nyingi hujiweka kama kiongozi na kuchukua wajibu wa kielelezo cha haki. Akisingizia kuwa anasalimisha haki, anaishia kumdhuru binadamu, kudanganya nafsi zao, na kutumia mbinu zote ili kuweza kuteka nyara hisia na fikira za binadamu, kumdanganya na kumchochea. Shabaha yake ni kumfanya binadamu kuidhinisha na kuufuata mwenendo wake wa maovu, kumfanya binadamu kujiunga naye katika kupinga mamlaka na ukuu wa Mungu. Hata hivyo, wakati mtu anapokuwa mwerevu na kutambua njama zake, mipango na sifa zake hizo na hataki kuendelea kudhalilishwa na kudanganywa naye hivyo au kuendelea kuwa mtumwa wa Shetani, au kuadhibiwa na kuangamizwa pamoja na Shetani, Shetani naye hubadilisha sifa zake za awali za utakatifu na kuondoa baraka yake bandia ili kufichua uso wake wa kweli wenye maovu, ubaya, sura mbaya na wa kikatili. Shetani hawezi kupenda jambo lolote isipokuwa kumaliza wale wote wanaokataa kumfuata yeye na wale wanaopinga nguvu zake za giza. Wakati huu Shetani hawezi tena kuvaa

sura ya uaminifu, na utulivu; badala yake, sifa zake za kweli za sura mbaya na za kishetani zilizokuwa zimefichwa kwenye mavazi ya kondoo zinafichuliwa. Mara tu njama za Shetani zinapomulikwa, na sifa zake za kweli kufichuliwa, yeye huingia kwenye hisia za hasira kali na kuonyesha ushenzi wake; tamanio lake la kudhuru na kudanganya watu ndipo litazidi zaidi. Hii ni kwa sababu anapandwa na hasira kali kwa kuzindukana kwa binadamu; anataka kuwa na kisasi kingi dhidi ya binadamu kwa maazimio yake ya kutamani kuwa na uhuru na nuru na kutokuwa mateka wa jela yake. Hasira yake kali inanuiwa kutetea maovu yake, na pia ni ufunuo wa kweli wa asili yake ya kishenzi.

Katika kila suala, tabia ya Shetani hufichua asili yake maovu. Kati ya vitendo vyote vya maovu ambavyo Shetani ametekeleza kwa binadamu—kutoka kwa jitihada zake za mapema za kudanganya binadamu ili aweze kumfuata, hadi unyonyaji wake wa binadamu, ambapo anamkokota binadamu hadi kwenye matendo maovu, hadi ulipizaji wa kisasi wa Shetani kwa binadamu baada ya sifa zake za kweli kuweza kufichuliwa na binadamu kuweza kutambua na kumwacha—hakuna hata kimoja kati ya vitendo hivi kinachoshindwa kufichua hali halisi ya uovu wa Shetani; hakuna hata moja inayoshindwa kuthibitisha hoja kwamba Shetani hana uhusiano na mambo mazuri; hakuna hata moja hushindwa kuthibitisha kwamba Shetani ndiye chanzo cha mambo yote maovu. Kila mojawapo ya matendo yake inasalimisha maovu yake, inadumisha maendelezo ya vitendo vyake vya maovu, inaenda kinyume cha haki na mambo mazuri, inaharibu sheria na mpangilio wa uwepo wa kawaida wa binadamu. Wao ni katili kwa Mungu, na ndio wale ambao hasira ya Mungu itaangamiza. Ingawaje Shetani anayo hasira yake kali, hasira yake kali ni mbinu ya kutoa nje asili yake mbovu. Sababu inayomfanya Shetani kukereka na kuwa mkali ni: Kwa sababu njama zake zisizotamkika zimefichuliwa; mipango yake haikwepeki kwa urahisi; malengo yake yasiyo na mipaka na tamanio la kubadilisha Mungu na kujifanya kuwa Mungu, vyote vimekwama na kuzuiliwa; shabaha yake ya kudhibiti binadamu wote imeishia patupu na haiwezi tena kutimizwa. Kuitisha kwa Mungu hasira Yake mara kwa mara ndiko kumesitisha mipango ya Shetani dhidi ya kukamilika na kukatiza kuenea na kusambaa kwa maovu ya Shetani; kwa hivyo, Shetani anaogopa na kuchukia hasira ya Mungu. Kila matumizi ya hasira ya Mungu huwa yanafichua sura halisi ya aibu ya Shetani; na pia kufichua na kuweka kwenye nuru matamano ya maovu ya Shetani. Wakati uo huo, sababu za hasira kali ya Shetani dhidi ya binadamu zinafichuliwa kabisa. Kule kulipuka kwa hasira kali ya Shetani ni ufunuo wa kweli wa asili yake mbovu, ufichuzi wa njama zake. Bila shaka, kila wakati Shetani anapopandwa na hasira kali, huwa ni dalili ya maangamizo ya mambo maovu; huashiria ulinzi na mwendelezo wa mambo mazuri, na huashiria asili ya hasira ya Mungu—ile ambayo haiwezi kukosewa!

Mtu Hafai Kutegemea Uzoefu na Fikiria Ili Kujua Tabia ya Haki ya Mungu

Ukijipata unakabiliwa na hukumu na kuadibiwa na Mungu, je, utasema kwamba neno la Mungu limetiwa najisi? Je, utasema kwamba kunayo hadithi inayoelezea hasira kali ya Mungu, na kwamba hasira Yake kali imetiwa najisi? Je, utamchafulia Mungu jina, ukisema kwamba tabia Yake si ya haki kwa ujumla? Wakati unaposhughulikia kila mojawapo ya vitendo vya Mungu, lazima uwe na hakika kwamba tabia ya haki ya Mungu iko huru dhidi ya vipengele vingine vyovyote, kwamba ni takatifu na haina dosari; vitendo hivi vinajumuisha binadamu kuweza kuangushwa chini, kuadhibiwa na kuangamizwa na Mungu. Bila kuacha, kila kimojawapo cha vitendo vya Mungu kinatekelezwa kulingana na tabia yake ya asili na mpango Wake—hii haijumuishi maarifa ya binadamu, mila na falsafa—na kila kimojawapo cha vitendo vya Mungu ni maonyesho ya tabia Yake na hali halisi, isiyohusiana na chochote kinachomilikiwa na binadamu aliyepotoka. Katika dhana za binadamu, ni upendo, huruma na uvumilivu wa Mungu tu kwa binadamu ndivyo visivyokuwa na dosari, ambavyo havijatiwa najisi na vilivyo vitakatifu. Hata hivyo, hakuna anayejua kwamba ghadhabu ya Mungu na hasira Yake vilevile vyote havijatiwa najisi; aidha, hakuna yule aliyefikiria maswali kama vile: kwa nini Mungu havumilii kosa lolote au kwa nini ghadhabu Yake ni kubwa mno. Kinyume ni kwamba, baadhi ya watu hukosa kuelewa hasira ya Mungu na kudhania kuwa ni hasira kali ya binadamu waliopotoka: wanaelewa ghadhabu ya Mungu kuwa hasira kali ya binadamu waliopotoka; wao hata hudhania kimakosa kwamba hasira kali ya Mungu ni sawa tu na ufunuo wa kiasili wa tabia potovu ya binadamu. Wanasadiki kimakosa kwamba utoaji wa hasira ya Mungu ni sawa tu na ghadhabu ya binadamu waliopotoka, jambo linalotokana na kutoridhika; wanasadiki hata kwamba utoaji wa hasira ya Mungu ni maonyesho ya hali Yake ya moyo. Baada ya kikao hiki cha ushirika, Ninatumai kwamba kila mmoja wenu hatakuwa tena na dhana potovu, fikira au kukisia kuhusiana na tabia ya haki ya Mungu, na Natumai baada ya kusikiliza maneno Yangu mnaweza kuwa na utambuzi wa kweli wa hasira ya tabia ya haki ya Mungu katika mioyo yenu, kwamba mnaweza kuweka pembeni kuelewa kokote kwa awali kulikofikiriwa vinginevyo kuhusiana na hasira ya Mungu, kwamba mnaweza kubadilisha imani zenu binafsi zilizopotoka na mitazamo ya hali halisi ya hasira ya Mungu. Vilevile, Natumai kwamba mnaweza kuwa na ufafanuzi sahihi wa tabia ya Mungu katika mioyo yenu, kwamba hamtakuwa tena na mashaka yoyote kuhusiana na tabia ya haki ya Mungu, na kwamba hamtatumia kuwaza kokote kwa binadamu au kufikiria kuhusu tabia ya kweli ya Mungu. Tabia ya haki ya Mungu ni hali halisi ya kweli ya Mungu mwenyewe. Si kitu kilichotungwa au kuandikwa na binadamu. Tabia Yake ni tabia Yake ya haki na haina uhusiano au miunganisho yoyote na uumbaji wowote ule. Mungu Mwenyewe ni Mungu Mwenyewe. Hatawahi kuwa sehemu ya uumbaji, na hata kama Atakuwa mwanachama miongoni mwa viumbe vilivyoyumbwa, tabia Yake ya asili na hali halisi Yake havitabadilika. Hivyo basi, kumjua Mungu si kujua kifaa; si kuchunguza kitu, wala si kuelewa mtu. Kama mwanadamu atatumia dhana au mbinu yake ya kujua kifaa au kuelewa mtu ili

kumjua Mungu, basi hutawahi kuweza kutimiza maarifa ya Mungu. Kumjua Mungu hakutegemei uzoefu au kufikiria kwako, na hivyo basi hufai kulazimisha uzoefu wako au kufikiria kwako kwa Mungu. Haijalishi uzoefu au kufikiria kwako ni kwa kipekee namna gani, huko kote bado ni finyu; na hata zaidi, kufikiria kwako hakulingani na hoja, isitoshe hakulingani na ukweli, na pia hakulingani na tabia na hali halisi ya kweli ya Mungu. Hutawahi kufanikiwa kama utategemea kufikiria kwako ili kuelewa hali halisi ya Mungu. Njia ya pekee ni hivi: kukubali yote yanayotoka kwa Mungu, kisha kwa utaratibu uweze kuyapitia na kuyaelewa. Kutakuwa na siku ambayo Mungu atakupa nuru ili uweze kuelewa kwa kweli na kumjua Yeye kwa sababu ya ushirikiano wako na kwa sababu ya hamu yako ya kutaka ukweli. Na kwa haya, hebu na tuhitimishe sehemu hii ya mazungumzo yetu.

Binadamu Hupata Huruma na Uvumilivu wa Mungu Kupitia kwa Toba ya Dhati

Kinachofuata ni hadithi ya biblia ya “Wokovu wa Mungu kwa Ninawi.”

Yona 1:1-2 Sasa neno la Yehova likaja kwa Yona mwana wa Amitai, likisema, Amka, nenda Ninawi, mji mkuu, na uipigie kelele, kwani uovu wao umeenda juu mbele Yangu.

Yona 3 Neno lake Yehova likakuja kwake Yona kwa mara ya pili, likisema, Inuka, nenda Ninawi, mji huo mkuu; na uhubirie mahubiri ninayokuambia. Kwa hivyo Yona akainuka, na kuenda Ninawi, kulingana na neno la Yehova. Sasa Ninawi ulikuwa mji mkuu wa safari ya siku tatu. Naye Yona akaanza kuingia ndani ya mji huo safari ya siku moja, na akatoa sauti kubwa, na kusema, Imebaki siku arobaini, na Ninawi utashindwa. Basi watu wa hapo Ninawi wakamwamini Mungu, na wakatangaza mfungo, na wakavalia nguo za magunia, kuanzia aliyekuwa mkubwa zaidi kwao mpaka aliyekuwa mdogo zaidi. Kwa kuwa habari ilimfikia mfalme wa Ninawi, na akainuka kutoka kwa kiti chake che enzi, na akaivua nguo yake, na kuvaa nguo ya gunia, na kukaa chini katika majivu. Na akafanya kutangazwe Ninawi kupitia amri yake mfalme na wakubwa wake, ikisema, Mtu wala mnyama, wala kundi la ng'ombe, wala kundi la kondoo wasionje chochote: wasikule, wala kunywa maji: Ila mwanadamu na mnyama wavikwe kwa nguzo za magunia, na kulia kwa nguvu kwa Mungu: ndiyo, na wawageuze watu wote kutoka kwa njia ovu, na kutoka kwa vurugu iliyo mikononi mwao. Nani anayejua iwapo Mungu atabadili na kughairi, na kuiacha ghadhabu Yake iliyo kali, ili tusingamie? Naye Mungu aliona vitendo vyao, kwamba walikuwa wameiacha njia yao ovu; na Mungu akaghairi lile neno ovu, ambalo Alikuwa amesema Angeliwafanyia; na Aakulifanya.

Yona 4 Lakini lilimwudhi Yona mno, naye alikuwa na hasira sana. Na akaomba kwa Yehova, na kusema, Nakuomba, Ee Yehova, hivi sivyo nilivyonena, nilipokuwa bado katika nchi yangu? Kwa hivyo nilitorokea Tarshishi kabla: kwa sababu nilijua kwamba Wewe ni Mungu wa

neema, na mwenye huruma, asiyekasirika haraka, na wa rehema kubwa, na Wewe unaghairi maovu. Kwa hivyo sasa, Ee Yehova, chukua, nakusihi, uhai wangu kutoka kwangu; kwa sababu ni heri nikufe kuliko kuishi. Kisha Yehova akasema, Je, unafanya vizuri kukasirika? Hivyo Yona akatoka nje ya mji, na kuketi katika upande wa mashariki wa mji, na huko akajitengenezea kibanda, na akaketi chini yake katika kivuli, mpaka aweze kuona kile kingefanyikia mji huo. Naye Yehova Mungu akatayarisha mtango, na akaufanya ukuje juu yake Yona, ili uweze kuwa kivuli juu ya kichwa chake, na kumwokoza kutoka katika huzuni yake. Kwa hivyo Yona akawa na furaha sana juu ya ule mtango. Lakini Mungu akatayarisha buu siku iliyofuata wakati kulipopambazuka, nalo likaula ule mtango hadi ukanyauka. Na hivyo ikatimia, wakati jua lilipopanda, kwamba Mungu akautayarisha upepo mkali wa mashariki; na jua likapiga kichwa chake Yona, kiasi kwamba alizimia, naye akatamani afe, na akasema, Ni heri mimi nife kuliko niishi. Mungu akasema kwa Yona, Je, unafanya vizuri kukasirika kwa sababu ya mtango? Na yeye akasema, naam, nafanya vizuri kukasirika, hata mpaka kufa. Kisha Yehova akasema, Umeuonea mtango huruma, ambao hujafanyia kazi, wala kuukuza; ambao ulimea kwa usiku mmoja, na kufa kwa usiku mmoja: Nami sipaswi kuonea Ninawi huruma, mji ule mkuu, ulio na zaidi ya watu elfu mia na ishirini ndani yake ambao hawawezi kutambua kati ya mkono wao wa kulia na mkono wao wa kushoto; na pia mifugo wengi?

Muhtasari wa Hadithi ya Ninawi

Ingawaje hadithi ya “wokovu wa Mungu wa Ninawi” ni fupi kwa urefu, inaruhusu mtu kuweza kuona kidogo tu ule upande mwingine wa tabia ya haki ya Mungu. Ili kuweza kuelewa haswa upande huo unajumuisha nini, lazima turudi kwenye Maandiko na kuangalia nyuma katika mojawapo ya matendo ya Mungu.

Hebu kwanza tuangalie mwanzo wa hadithi hii: “Sasa neno la Yehova likaja kwa Yona mwana wa Amitai, likisema, Amka, nenda Ninawi, mji mkuu, na uipigie kelele, kwani uovu wao umeenda juu mbele Yangu” (Yona 1:1-2). Katika fungu hili kutoka kwenye Maandiko, tunajua kwamba Yehova Mungu alimwamuru Yona kwenda katika mji wa Ninawi. Kwa nini alimwamuru Yona kwenda katika mji huo? Biblia iko wazi kabisa kuhusu suala hili: Maovu ya watu walio ndani ya mji huo yalikuwa yamefikia macho ya Yehova Mungu, na hivyo basi Alimtuma Yona ili kuwatangazia kile Alichonuia kufanya. Ingawa hakuna kitu kilichorekodiwa kinachotwambia Yona alikuwa nani, jambo hili, bila shaka, halina uhusiano wowote na kumjua Mungu. Hivyo basi, huhitaji kumwelewa mwanamume huyu. Unahitaji kujua tu kile ambacho Mungu alimwamuru Yona kufanya na kwa nini Alifanya kitu hicho.

Onyo la Yehova Mungu Lawafikia Waninawi

Hebu tuendeleo hadi kwenye fungu la pili, sura ya tatu ya kitabu cha Yona: “Naye Yona akaanza kuingia ndani ya mji huo safari ya siku moja, na akatoa sauti kubwa, na kusema, Imebaki siku arobaini, na Ninawi utashindwa.” Haya ndiyo maneno ambayo Mungu alipitisha moja kwa moja kwake Yona ili aweze kuwaambia Waninawi. Ndiyo pia, kwa kawaida, maneno ambayo Yehova alipenda kusema kwa Waninawi. Maneno haya yanatwambia kwamba Mungu alianza kukerwa na kuchukia watu wa mji huu kwa sababu ya maovu yao yaliyokuwa yamefika machoni pa Mungu, na hivyo basi, Alipenda kuuangamiza mji huo. Hata hivyo, kabla ya Mungu kuangamiza mji, Aliwatangazia Waninawi, na hapo kwa hapo Akawapa fursa ya kutubu maovu yao na kuanza upya. Fursa hii ingedumu kwa siku arubaini. Kwa maneno mengine, kama watu waliokuwa ndani ya mji huu wasingetubu, na kukubali dhambi au maovu yao wenyewe mbele ya Yehova Mungu ndani ya siku arubaini, Mungu angeangamiza mji huu kama Alivyoangamiza Sodoma. Hivi ndivyo ambavyo Yehova Mungu alipenda kuwaambia watu wa Ninawi. Ni wazi kwamba, hili halikuwa tangazo rahisi. Halikuweza tu kuonyesha hasira ya Yehova Mungu, lakini pia lilionyesha mtazamo Wake kwa wale Waninawi; wakati uo huo tangazo hili rahisi lilitumika kama onyo kali kwa watu waliokuwa wakiishi ndani ya mji huo. Onyo hili liliwaambia kwamba matendo yao maovu yalikuwa yamewafanya kuchukiwa na Yehova Mungu na liliwaambia kwamba matendo yao maovu yanguwaletea hivi karibuni fedheha kutokana na maangamizo yao wenyewe; kwa hivyo, maisha ya kila mmoja kule Ninawi yalikuwa karibu kuangamia.

Utufautishaji Mkavu Katika Mwitikio wa Ninawi na Sodoma kwa Onyo la Yehova Mungu

Kupinduliwa kunamaanisha nini? Kwa muktadha wa mazungumzo, kunamaanisha kutoweka. Lakini kwa njia gani? Ni nani angefanya mji mzima kupinduliwa? Haiwezekani kwa binadamu kufanya kitendo kama hicho, bila shaka. Watu hawa hawakuwa wajinga; mara tu waliposikia matangazo haya, walipata wazo hilo. Walijua kwamba yalikuwa yametoka kwa Mungu; walijua kwamba Mungu angetekeleza kazi Yake; walijua kwamba maovu yao yalikuwa yamemkasirisha Yehova Mungu na kumfanya kuwa na hasira kali kwao, ili waweze kuangamizwa pamoja na mji wao. Je, watu wa mji huo walichukulia vipi suala hilo baada ya kusikiliza onyo la Yehova Mungu? Biblia inafafanua kwa maelezo fafanuzi namna ambavyo watu hawa walivyoitikia, kuanzia kwa mfalme wao hadi kwa binadamu wa kawaida. Kama ilivyorekodiwa kwenye Maandiko: “Basi watu wa hapo Ninawi wakamwamini Mungu, na wakatangaza mfungo, na wakavalia nguo za magunia, kuanzia aliyekuwa mkubwa zaidi kwao mpaka aliyekuwa mdogo zaidi. Kwa kuwa habari ilimfikia mfalme wa Ninawi, na akainuka kutoka kwa kiti chake che enzi, na akaivua nguo yake, na kuvaa nguo ya gunia, na kukaa chini katika majivu. Na akafanya kutangazwe Ninawi kupitia amri yake mfalme na wakubwa wake, ikisema, Mtu wala mnyama, wala kundi la ng’ombe, wala kundi la kondoo wasionje chochote: wasikule, wala kunywa maji: Ila mwanadamu na mnyama wavikwe kwa nguzo za magunia, na

kulia kwa nguvu kwa Mungu: ndiyo, na wawageuze watu wote kutoka kwa njia ovu, na kutoka kwa vurugu iliyo mikononi mwao. ...”

Baada ya kusikia tangazo la Yehova Mungu, watu wa Ninawi walionyesha mtazamo uliokuwa kinyume kabisa na ule wa watu wa Sodoma—watu wa Sodoma walimpinga Mungu waziwazi, huku wakiendelea kutoka kwa maovu hadi maovu, lakini baada ya kusikia maneno haya, Waninawi hawakupuuza suala hilo, wala hawakuweza kulipinga; badala yake walimsadiki Mungu na kutangaza kufunga. “Walisadiki” inarejelea nini hapa? Neno lenyewe linapendekeza imani na unyenyekevu. Kama tutatumia tabia halisi ya Waninawi kuelezea neno hili, inamaanisha kwamba walisadiki Mungu anaweza na angeweza kufanya vile Alivyosema, na kwamba walikuwa radhi kutubu. Je, watu wa Ninawi walihisi woga mbele ya janga lililokuwa karibu kutokea? Imani yao ndiyo iliyotia woga katika mioyo yao. Kwa kweli, ni nini tunachoweza kutumia kuthibitisha Imani na woga wa Waninawi? Ni sawa na vile Biblia inavyosema: “na wao wakatangaza kufunga, na wakavalia nguo ya gunia, kuanzia wale walio wakubwa zaidi na hata kwa wale walio wadogo zaidi.” Hivi ni kusema kwamba Waninawi walisadiki kweli, na kwamba kutoka kwenye imani hii woga uliibuka, ambao sasa ulisababisha kufunga na kuvaliwa kwa nguo ya gunia. Hivi ndivyo walivyoonyesha mwanzo wa toba yao. Tofauti kabisa na watu wa Sodoma, Waninawi hawakumpinga Mungu tu, bali walionyesha pia waziwazi toba yao kupitia kwa tabia na matendo yao. Bila shaka, hii haikutumika tu kwa watu wa kawaida wa Ninawi; hata mfalme wao hakubakizwa.

Toba ya Mfalme wa Ninawi Inapata Sifa ya Yehova Mungu

Wakati mfalme wa Ninawi alipozisikia habari hizi, aliinuka kutoka kwenye kiti chake cha enzi, akavua nguo zake, akavalia nguo ya gunia na kukalia jivu. Kisha akatangaza kwamba hakuna mtu kwenye mji huo ambaye angeruhusiwa kuonja chochote, na kuwa hakuna mifugo, wanakondoo na ng’ombe ambao wangekunywa maji na kula nyasi. Binadamu na mifugo kwa pamoja walitakikana kujifunika nguo ya gunia; nao watu wangemsihi Mungu kwa uaminifu. Mfalme pia alitangaza kwamba watu wote wangetupilia mbali njia zao za maovu na kukataa udhalimu ulioko mikononi mwao. Tukifanya uamuzi kutoka kwenye misururu ya vitendo hivi, mfalme wa Ninawi alionyesha toba yake ya dhati. Misururu ya vitendo alivyofanya—kutoka kwenye kiti chake cha ufalme, kulitupa joho lake la kifalme, kuvalia nguo ya gunia na kukalia majivu—kulionyesha watu kwamba mfalme wa Ninawi aliweka kando hadhi yake ya kifalme na kuvalia nguo ya gunia pamoja na watu wa kawaida wa nchi. Hii ni kusema kwamba mfalme wa Ninawi hakuweza kushikilia wadhifa wake wa kifalme ili aendelee na njia zake za maovu au udhalimu katika mikono yake baada ya kikao cha tangazo kutoka kwa Yehova Mungu; badala yake, aliweka pembeni mamlaka aliyoyashikilia na kutubu mbele ya Yehova Mungu. Kwenye

kipindi hiki cha muda, mfalme wa Ninawi hakuwa akitubu akiwa mfalme; alikuwa amekuja mbele ya Mungu kuungama na kutubu dhambi zake akiwa binadamu wa kawaida wa Mungu. Aidha, aliuambia mji mzima kuungama na kutubu dhambi zao mbele ya Yehova Mungu kwa njia sawa na yeye; vilevile, alikuwa na mpango mahususi wa namna ya kufanya hivyo kama inavyoonekana kwenye Maandiko: “Mtu wala mnyama, wala kundi la ng’ombe, wala kundi la kondoo wasionje chochote: wasikule, wala kunywa maji: ... na kulia kwa nguvu kwa Mungu: ndiyo, na wawageuze watu wote kutoka kwa njia ovu, na kutoka kwa vurugu iliyo mikononi mwao.” Kama kiongozi wa mji, mfalme wa Ninawi alimiliki hadhi na nguvu za kimamlaka na angefanya chochote alichopenda. Alipokabiliwa na tangazo la Yehova Mungu, angeweza kupuuza suala hilo au kutubu na kuungama tu dhambi zake pekee; kuhusiana na kama watu wa mji wangepuuza kutubu au la, angepuuza suala hili kabisa. Hata hivyo, mfalme wa Ninawi hakufanya hivyo kamwe. Mbali na kuinuka kutoka kwenye kiti chake cha enzi, kuvalia nguo ya gunia na kujipaka jivu na kuungama na kutubu dhambi zake mbele ya Yehova Mungu, aliweza pia kuwaamuru watu na mifugo ndani ya mji huo kufanya hivyo. Aliweza hata kuamuru watu “kumlilia Mungu kwa nguvu.” Kupitia misururu hii ya vitendo, mfalme wa Ninawi aliweza kukamilisha kwa kweli kile ambacho kiongozi anafaa kufanya; misururu ya vitendo vyake ndiyo iliyokuwa migumu kwa mfalme yeyote katika historia ya binadamu kutimiza, hatua na pia hatua ambayo hakuna aliyewahi kutimiza. Matendo haya yanaweza kuitwa shughuli isiyo na kifani katika historia ya binadamu; yanastahili kukumbukwa na kuigwa na binadamu. Tangu enzi ya mwanadamu, kila mfalme alikuwa amewaongoza wafuasi wake kukinzana na kumpinga Mungu. Hakuna yule aliyewahi kuwaongoza wafuasi wake kusihi Mungu kutafuta ukombozi kwa ajili ya maovu yao, kupokea msamaha wa Yehova Mungu na kuepuka adhabu kali. Mfalme wa Ninawi, hata hivyo, aliweza kuwaongoza raia wake kumlilia Mungu, kuacha njia zao mbalimbali za maovu na kutupilia mbali udhalimu ulio mikononi mwao. Aidha, aliweza pia kuweka kando kiti chake cha enzi, na badala yake, Yehova Mungu alibadilisha na kughairi na kugeuza hasira Yake, na kuruhusu watu wa mji huu kuishi na kuwalinda dhidi ya kuangamia. Matendo ya mfalme yanaweza kuitwa tu muujiza wa nadra katika historia ya binadamu; yanaweza hata kuitwa kielelezo cha binadamu uliopotoka unaoungama na kutubu dhambi zake mbele ya Mungu.

Mungu Aona Kutubu kwa Dhati katika Vina vya Mioyo ya Waninawi

Baada ya kusikiliza tangazo la Mungu, mfalme wa Ninawi na raia Wake walitekeleza misururu ya vitendo. Je, ni nini asili ya tabia na matendo yao? Kwa maneno mengine, ni nini kiini cha uzima wa mwenendo wao? Kwa nini walifanya kile walichofanya? Katika macho ya Mungu walikuwa wametubu kwa dhati, si tu kwa sababu walikuwa wamemsihi Mungu kwa dhati na kuungama dhambi zao mbele Yake, lakini pia kwa sababu walikuwa wameacha mwenendo wao wenye maovu. Walichukua hatua namna hii kwa sababu baada ya kusikia

matamshi ya Mungu, walitishika pakubwa na kusadiki kwamba angefanya vile ambavyo alikuwa amesema. Kwa kufunga, kuvalia nguo ya gunia na kukalia jivu, walipenda kuonyesha namna walivyokuwa radhi kubadilisha njia zao na kujizuia na maovu, kumwomba Yehova Mungu kuzuia hasira Yake, kusihi Yehova Mungu kutupilia mbali uamuzi Wake, pamoja na msiba mkuu ambao ulikuwa karibu kuwasibu. Kupitia uchunguzi wa tabia yao yote, tunaona ya kwamba tayari walielewa kwamba vitendo vyao vya awali vilimchukiza Yehova Mungu na kwamba walielewa sababu iliyomfanya kutaka kuwaangamiza hivi karibuni. Kwa sababu hizi, wote walipenda kutubu kabisa, kugeuka na kuacha njia zao za maovu na kuacha udhalimu ulio mikononi mwao. Kwa maneno mengine, pindi tu walipotambua tangazo la Yehova Mungu, kila mmoja wao alihisi woga katika mioyo yao; hawakuendelea tena na mwenendo wao wa maovu wala kuendelea kutenda vitendo ambavyo Yehova Mungu alichukia. Vilevile, walimsihi Yehova Mungu kusamehe dhambi zao za kale na kutowatendea kulingana na vitendo vyao vya kale. Walikuwa radhi kutowahi kujihusisha tena katika maovu na kutenda kulingana na maagizo ya Yehova Mungu, kama tu wasingewahi kumkasirisha Yehova Mungu. Toba yao ilikuwa ya dhati na ya kweli. Ilitoka kwenye kina cha mioyo yao na haikuwa ya kujidanganya, wala haikuwa ya muda.

Baada ya watu wa Ninawi, kutoka kwa mfalme mwenye mamlaka hadi kwa raia wake, kujua kwamba Yehova Mungu alikuwa amewakasirikia, kila mojawapo ya vitendo vyao, tabia yao nzima, pamoja na kila mojawapo ya uamuzi na machaguo yao vilikuwa wazi na dhahiri mbele ya Mungu. Moyo wa Mungu ulibadilika kulingana na tabia yao. Akili Zake Mungu zilikuwa zinafikiria nini wakati huo? Biblia inaweza kukujibia swali hili. Maneno yafuatayo yalirekodiwa katika maandiko: “Naye Mungu aliona vitendo vyao, kwamba walikuwa wameiacha njia yao ovu; na Mungu akaghairi lile neno ovu, ambalo Alikuwa amesema Angeliwafanyia; na Hakulifanya.” Ingawaje Mungu alibadilisha fikira Yake, hakukuwa na chochote kigumu kuhusu mtazamo wa fikira Yake. Aliweza kubadilika kutoka katika kuonyesha hasira Yake hadi kutuliza hasira Yake, na kisha kuamua kutouleta msiba mkuu katika mji wa Ninawi. Sababu ya uamuzi wa Mungu wa—kuwaokoa Waninawi dhidi ya msiba wao mkuu—ilikuwa ya haraka mno, ni kwa sababu Mungu aliangalia moyo wa kila mmoja wa wale Waninawi. Aliona kwamba katika kina cha mioyo yao waliweza: kuungama na kutubu kwa dhati dhambi zao, imani yao ya dhati kwake Yeye, mtazamo wao wa kina kuhusu vile vitendo vyao vya maovu vilikuwa vimeipa tabia Yake hasira kali, na woga uliotokana na adhabu ya Yehova Mungu iliyokuwa inakaribia. Wakati uo huo, Yehova Mungu aliweza kusikia maombi kutoka kwenye kina cha mioyo yao wakimsihi kusitisha hasira Yake dhidi yao ili waweze kuepuka msiba huu mkuu. Wakati Mungu alipoangalia hoja hizi zote, kwa utaratibu hasira yake ilitoweka. Licha ya vile hasira yake ilivyokuwa kuu hapo awali, alipoona kutubu kwao kwa dhati ndani ya

kina cha mioyo ya watu hawa, moyo Wake uliguswa na hili, na kwa hivyo Hakuweza kuvumilia kuwaletea msiba mkuu, na Alisitisha hasira yake kwao. Badala yake Aliendelea kuwaonyesha huruma Yake na uvumilivu kwao na akaendelea kuwaongoza na kuwakimu.

Kama Imani Yako kwa Mungu ni ya Kweli, Utapokea Utunzaji Wake Mara Nyingi

Mungu kubadilisha nia Zake kwa watu wa Ninawi hakukuhusisha kusitasita au kutoeleweka kokote. Badala yake kulikuwa ni mabadiliko kutoka kwa hasira tupu hadi uvumilivu mtupu. Huu ni ufunuo wa kweli wa kiini cha Mungu. Mungu kamwe si wa kusitasita au asiye na uamuzi katika vitendo Vyake; kanuni na makusudio yaliyo katika matendo Yake yote ni wazi na dhahiri, yasiyo na dosari wala doa, yasiyo kabisa na hila ama njama zozote zilizochanganywa ndani. Kwa maneno mengine, kiini cha Mungu hakina giza wala maovu. Mungu alikasirikia Waninawi kwa sababu vitendo vyao viovu vilikuwa vimefikia macho Yake; wakati ule hasira Yake ilitokana na kiini Chake. Hata hivyo, wakati hasira ya Mungu ilitoweka na akatoa uvumilivu Wake kwa watu wa Ninawi kwa mara nyingine tena, kila kitu Alichofichua kilikuwa bado ni kiini Chake. Uzima wa badiliko hili ulitokana na badiliko katika mtazamo wa mwanadamu kwa Mungu. Katika kipindi hiki chote cha muda, tabia ya Mungu isiyokosewa haikubadilika; kiini cha Mungu cha uvumilivu hakikubadilika; kiini cha Mungu cha upendo na huruma hakikubadilika. Wakati watu wanapotekeleza vitendo viovu na kumkosea Mungu atawashushia ghadhabu Yake. Wakati watu wanatubu kwa kweli, moyo wa Mungu utabadilika, na hasira Yake itakoma. Wakati watu wanapoendelea kumpinga Mungu kwa ukaidi, hasira Yake kali haitakoma; hasira Yake itawalemea hatua kwa hatua mpaka watakapoangamizwa. Hiki ndicho kiini cha tabia ya Mungu. Haijalishi kama Mungu anaonyesha hasira au huruma na wema, mwenendo wa binadamu, tabia na mtazamo wake kwa Mungu ndani ya kina cha moyo wake vinaamrisha kile ambacho kinaonyeshwa kupitia kwa ufunuo wa tabia ya Mungu. Kama Mungu anaendelea kumfanya mtu apitie hasira Yake, moyo wa mtu huyu bila shaka humpinga Mungu. Kwa sababu hajawahi kutubu kwa kweli, kuinamisha kichwa chake mbele ya Mungu au kumiliki imani ya kweli kwa Mungu, hajawahi kupata huruma na uvumilivu wa Mungu. Kama mtu hupokea utunzaji wa Mungu mara nyingi na hupokea huruma na uvumilivu Wake mara nyingi, basi mtu huyo bila shaka anaamini Mungu kwa kweli ndani ya moyo wake, na moyo wake haumpingi Mungu. Yeye kwa mara nyingi anatubu kwa kweli mbele ya Mungu; kwa hivyo, hata kama nidhamu ya Mungu mara nyingi humshukia mtu huyu, hasira Yake haitamshukia.

Maelezo haya mafupi yanaruhusu watu kuuona moyo wa Mungu, kuona uhalisi wa kiini Chake, kuona kwamba ghadhabu ya Mungu na mabadiliko katika moyo Wake yana sababu. Licha ya utofautishaji mkavu ambao Mungu alionyesha Alipoghadhabishwa na wakati Alipobadilisha moyo Wake, jambo ambalo linafanya watu kusadiki kwamba utofautishaji mkavu

au nafasi kubwa yaonekana kuwepo kati ya vipengele hivi viwili vya kiini cha Mungu—ghadhabu Yake na uvumilivu Wake—mtazamo wa Mungu kwa kule kutubu kwa Waninawi kwa mara nyingine kunaruhusu watu kuweza kuona ule upande mwingine wa tabia halisi ya Mungu. Mabadiliko katika moyo wa Mungu yanaruhusu kwa kweli binadamu kwa mara nyingine kuuona ukweli wa huruma na wema wa Mungu na kuona ufunuo wa kweli wa kiini cha Mungu. Binadamu hawana budi kutambua kwamba rehema ya Mungu na wema si hadithi za uwongo tu, wala si ughushi. Hii ni kwa sababu hisia za Mungu kwa wakati huo zilikuwa kweli; Mabadiliko ya moyo wa Mungu yalikuwa kweli; Mungu kwa kweli aliwapa binadamu kwa mara nyingine tena rehema na uvumilivu Wake.

Toba ya Kweli Ndani ya Mioyo ya Waninawi Inawapa Rehema ya Mungu na Kubadilisha Hatima Zao Wenyewe

Je, kulikuwa na ukinzani wowote kati ya mabadiliko ya moyo wa Mungu na hasira Yake? Bila shaka la! Hii ni kwa sababu uvumilivu wa Mungu wakati ule maalum ulikuwa na sababu yake. Je, sababu yake yaweza kuwa nini? Ni ile iliyotolewa katika Biblia: “Kila mtu aligeuka kutoka kwenye njia yake ovu” na “kuacha vurugu iliyokuwa mikononi mwake.”

Hii “nvia ovu” hairejelei kiasi kidogo cha vitendo viovu, lakini inarejelea chanzo cha maovu katika tabia ya watu. “Kugeuka kutoka njia yake ovu” kunamaanisha kwamba wale wanaozungumziwa hawatawahi kutekeleza vitendo hivi tena. Kwa maneno mengine, hawatawahi kutenda kwa njia hii ovu tena; mbinu, chanzo, kusudio, nia na kanuni za vitendo vyao vyote vimebadilika; hawatawahi tena kutumia mbinu na kanuni hizi kuleta nafuu na furaha mioyoni mwao. Kule “kuacha” katika “kuacha vurugu iliyo mikononi mwake” kunamaanisha kuweka chini au kuweka pembeni, kujitenga kabisa na mambo ya kale na kutorudi nyuma tena. Wakati watu wa Ninawi walipoacha vurugu iliyokuwa mikononi mwao, hii ilithibitisha na vilevile iliwakilisha toba yao ya kweli. Mungu huangalia kwa makini sehemu ya nje ya watu na vilevile mioyo yao. Wakati Mungu alipoangalia kwa makini toba ya kweli katika mioyo ya Waninawi bila kuuliza swali na pia kutambua kwamba walikuwa wameacha njia zao ovu na kuacha vurugu iliyokuwa mikononi mwao, Alibadilisha moyo Wake. Hivi ni kusema kwamba mwenendo na tabia ya watu hawa na njia mbalimbali za kufanya mambo, pamoja na ungamo na toba ya dhambi ya kweli zilizokuwa mioyoni mwao, kulisababisha Mungu kubadilisha moyo Wake, kubadilisha nia Zake, kufuta uamuzi Wake na kutowaadhibu wala kuwaangamiza. Kwa hivyo, watu wa Ninawi waliweza kufikia hatima tofauti. Waliyakomboa maisha yao binafsi na wakati uo huo wakupata huruma na uvumilivu wa Mungu, na wakati huo Mungu pia alifuta hasira Yake.

Huruma na Uvumilivu wa Mungu si Nadra—Toba ya Kweli ya Mwanadamu Ndiyo Nadra

Licha ya vile ambavyo Mungu alikuwa na ghadhabu kwa Waninawi, mara tu walipotangaza kufunga na kuvalia nguo ya gunia pamoja na jivu, moyo Wake ulianza kutulia taratibu, na Akaanza kubadilisha moyo Wake. Wakati Alipowatangazia kwamba Angeangamiza mji wao—ule muda kabla ya kuungama na kutubu kwao kwa dhambi zao—Mungu alikuwa angali na ghadhabu na wao. Baada ya wao kupitia mfululizo wa vitendo vya kutubu, ghadhabu ya Mungu kwa watu wa Ninawi ikabadilika kwa utaratibu kuwa huruma na uvumilivu kwao. Hakuna kitu kinachohitilafiana kuhusu ufunuo wenye ulinganifu wa vipengele hivi viwili vya tabia ya Mungu katika tukio lilo hilo. Ni vipi ambavyo mtu anafaa kuelewa na kujua ukosefu huu wa kuhitilafiana? Mungu alionyesha na kufichua viini hivi viwili tofauti kabisa kwa mfululizo wakati watu wa Ninawi walipokuwa wakitubu na Akawaruhusu watu kuona uhalisi na kutokosewa kwa kiini cha Mungu. Mungu alitumia mtazamo Wake kuambia watu yafuatayo: Si kwamba Mungu havumilii watu, au hataki kuwaonyesha huruma; ni kwamba wao hutubu kwa kweli mara nadra kwa Mungu, na ni nadra kwa watu kugeuka kwa kweli kutoka kwa njia zao ovu na kuacha vurugu iliyo mikononi mwao. Kwa maneno mengine, wakati Mungu ameghadhabishwa na binadamu, Anatumaini kwamba binadamu ataweza kutubu kwa kweli na Anatumaini kumwona binadamu akitubu kwa kweli, ambapo Ataendelea kumpa binadamu huruma na uvumilivu Wake kwa ukarimu. Hivi ni kusema kwamba mwenendo mbovu wa mwanadamu ndio husababisha hasira ya Mungu, huku nazo rehema na uvumilivu wa Mungu zikipewa wale wanaomsikiliza Mungu na kutubu kwa kweli mbele Yake, kwa wale wanaoweza kugeuka kutoka kwa njia zao ovu na kuacha vurugu iliyo mikononi mwao. Mtazamo wa Mungu ulifichuliwa waziwazi sana katika jinsi Alivyowatendea Waninawi: Huruma na uvumilivu wa Mungu si vigumu kuvipokea hata kidogo; Anahitaji toba ya kweli ya mtu. Mradi tu watu wageuka kutoka kwa njia zao ovu na kuuacha vurugu iliyo mikononi mwao, Mungu atabadilisha moyo Wake na kubadilisha mtazamo Wake kwao.

Tabia ya Haki ya Muumba ni ya Kweli na Wazi

Wakati Mungu alibadilisha moyo Wake kwa minajili ya watu wa Ninawi, je, huruma na uvumilivu Wake ulikuwa wa bandia? Bila shaka la! Basi mabadiliko kati ya vipengele hivi viwili vya tabia ya Mungu katika suala lili hili yanakuruhusu kuona nini? Tabia ya Mungu ni kamili kabisa; haijagawanywa hata kidogo. Licha ya kama Anaonyesha ghadhabu au huruma na uvumilivu kwa watu, haya yote ni maonyesho ya tabia Yake ya haki. Tabia ya Mungu ni kweli na wazi. Yeye hubadilisha fikira na mitazamo Yake kulingana na maendeleo ya mambo. Mabadiliko ya mtazamo Wake kwa Waninawi yanawaambia binadamu kwamba Anazo fikira na mawazo Yake mwenyewe; Yeye si roboti au sanamu ya udongo, bali Yeye ni Mungu Mwenyewe mwenye uhai. Angeweza kuwa na ghadhabu kwa watu wa Ninawi, sawa tu na vile ambavyo Angeweza kusamehe dhambi zao za kale kulingana na mitazamo yao; Angeweza

kuamua kuwaletea Waninawi msiba na Angeweza kubadilisha uamuzi Wake kwa sababu ya kutubu kwao. Watu hupenda kutumia sheria bila kupinda na kutumia sheria kama hizo ili kumwekea mipaka na kumfafanua Mungu, sawa tu na vile watu wanavyopendelea kutumia fomyula ili kujua tabia ya Mungu. Kwa hivyo, kulingana na himaya ya fikira za binadamu, Mungu hafikirii wala Yeye hana mawazo yoyote halisi. Kwa uhalisi, fikira za Mungu zinabadilika siku zote kulingana na mabadiliko katika mambo, na mazingira; huku fikira hizi zikiwa zinabadilika, vipengele tofauti vya kiini cha Mungu vitafichuliwa. Katika kipindi hiki cha mabadiliko, wakati ule Mungu hubadilisha moyo Wake, Yeye hufichulia mwanadamu ukweli wa uwepo wa maisha Yake na kufichua kwamba tabia Yake ya haki ni halisi na wazi. Aidha, Mungu hutumia ufunuo Wake mwenyewe wa kweli kuthibitisha kwa mwanadamu ukweli wa uwepo wa hasira Yake, huruma Yake, wema Wake na uvumilivu Wake. Kiini Chake kitafichuliwa wakati wowote na mahali popote kulingana na maendeleo ya mambo. Anamiliki hasira ya simba na huruma na uvumilivu wa mama. Tabia Yake ya haki hairuhusiwi kushukiwa, kukiukwa, kubadilishwa au kupotoshwa na mtu yeyote. Miongoni mwa masuala yote na mambo yote, tabia ya haki ya Mungu, yaani, hasira ya Mungu na huruma ya Mungu, vyote vinaweza kufichuliwa wakati wowote na mahali popote. Anaonyesha waziwazi vipengele hivi katika kila sehemu ya asili na kuzitekeleza kila wakati kwa uwazi. Tabia ya haki ya Mungu haiwekewi mipaka na muda au nafasi, au kwa maneno mengine, tabia ya haki ya Mungu haionyeshwi bila kufikiri au kufichuliwa kama inavyoongozwa na mipaka ya muda au nafasi. Badala yake, tabia ya haki ya Mungu inaonyeshwa kwa njia huru na kufichuliwa mahali popote na wakati wowote. Unapooni Mungu akibadilisha moyo Wake na kukoma kuonyesha hasira Yake na kujizuia dhidi ya kuuangamiza mji wa Ninawi, je, unaweza kusema kwamba Mungu ni mwenye huruma na upendo tu? Je, unaweza kusema kwamba hasira ya Mungu inajumuisha maneno matupu? Wakati Mungu anapoonyesha hasira kali na kuiondoa huruma Yake, je, unaweza kusema kwamba Hana hisia zozote za upendo wa kweli kwa binadamu? Mungu huonyesha hasira kali kutokana na vitendo viovu vya watu, hasira Yake haina kosa. Moyo wa Mungu unavutiwa na toba ya watu, na ni toba hii ambayo hubadilisha moyo Wake. Kuguswa kwake, mabadiliko katika moyo Wake pamoja na huruma na uvumilivu Wake kwa binadamu, vyote havina kosa kabisa; ni safi, havina kasoro, havina doa na havijachafuliwa. Uvumilivu wa Mungu ni uvumilivu mtupu; Huruma Yake ni huruma tupu. Tabia Yake itafichua hasira, pamoja na huruma na uvumilivu, kulingana na kutubu kwa binadamu na mwenendo wake tofauti. Haijalishi kile ambacho Anafichua na kuonyesha, yote hayo hayana kasoro; yote ni ya moja kwa moja; kiini Chake ni tofauti na chochote kile katika uumbaji. Kanuni za matendo ambazo Mungu huonyesha, fikira na mawazo Yake, au uamuzi wowote maalum, pamoja na kitendo chochote kimoja, vyote havina dosari wala doa. Kama jinsi ambavyo Mungu huamua na jinsi Atendavyo, ndivyo Anavyokamilisha shughuli Zake. Aina hizi za matokeo ni sahihi na hazina dosari kwa sababu chanzo chake hakina dosari na

doa lolote. Hasira ya Mungu haina dosari. Vilevile, huruma na uvumilivu wa Mungu, ambazo hazimilikiwi na kiumbe yeyote ni takatifu na hazina kosa, na zinaweza kustahimili fikira na uzoefu.

Baada ya kuelewa hadithi ya Ninawi, je, mnauona upande ule mwingine wa kiini cha tabia ya haki ya Mungu? Je, mnauona upande ule mwingine wa tabia ya haki na ya kipekee ya Mungu? Je, kunaye mtu yeyote miongoni mwa binadamu anayemiliki aina hii ya tabia? Je, kunaye mtu yeyote anayemiliki aina hii ya hasira kama ile ya Mungu? Je, kunaye mtu yeyote anayemiliki huruma na uvumilivu kama ule wa Mungu? Ni nani miongoni mwa viumbe anayeweza kuita hasira nyingi sana na kuamua kuangamiza au kuleta maafu kwa wanadamu? Na ni nani anazo sifa zinazostahili kutoa huruma kuvumilia na kumsamehe binadamu na hivyo basi kubadilisha uamuzi wake wa kuangamiza binadamu? Muumba huonyesha tabia Yake ya haki kupitia mbinu na kanuni Zake za binafsi za kipekee; Hategemei kudhibitiwa au kuzuiliwa na watu, matukio au mambo yoyote. Akiwa na tabia Yake ya kipekee, hakuna mtu anayeweza kubadilisha fikira na mawazo Yake, wala hakuna yule anayeweza kumshawishi Yeye na kubadilisha uamuzi wowote Wake. Uzima wa tabia na fikira za uumbaji upo katika hukumu ya tabia Yake ya haki. Hakuna anayeweza kudhibiti kama atatumia hasira au huruma; ni kiini cha Muumba tu—au kwa maneno mengine, tabia ya haki ya Muumba—kinaweza kuamua hili. Hii ndiyo asili ya kipekee ya tabia ya haki ya Muumba!

Baada ya kuchambua na kuelewa mabadiliko katika mtazamo wa Mungu kwa watu wa Ninawi, je, unaweza kutumia neno “upekee” kufafanua huruma inayopatikana katika tabia ya haki ya Mungu? Hapo awali tulisema kwamba hasira ya Mungu ni kipengele kimoja cha kiini cha tabia Yake ya haki na ya kipekee. Sasa Nitafafanua vipengele viwili, hasira ya Mungu na huruma ya Mungu, kama tabia Yake ya haki. Tabia ya haki ya Mungu ni takatifu; ni isiyokosewa pamoja na kushukiwa; ni kitu kisichomilikiwa na yeyote miongoni mwa viumbe vilivyoundwa au vile ambavyo havikuumbwa. Ni ya kipekee na maalum kwa Mungu pekee. Hivi ni kusema kwamba hasira ya Mungu ni takatifu na isiyokosewa Vivyo hivyo, kipengele kile kingine cha tabia ya haki ya Mungu—huruma ya Mungu—ni takatifu na haiwezi kukosewa. Hakuna yeyote kati ya viumbe vile vilivyoundwa au vile ambavyo havikuumbwa, anavyoweza kubadilisha au kuwakilisha Mungu katika vitendo Vyake, wala hakuna yeyote anayeweza kubadilisha au kumwakilisha Yeye katika kuangamiza Sodoma au wokovu wa Ninawi. Haya ndiyo maonyesho ya kweli ya tabia ya haki ya kipekee ya Mungu.

Hisia za Dhati za Muumba kwa Wanadamu

Watu mara nyingi husema kwamba si jambo rahisi kumjua Mungu. Mimi, hata hivyo, nasema kwamba kumjua Mungu si jambo gumu kamwe, kwani Mungu mara kwa mara huruhusu

binadamu kushuhudia matendo Yake. Mungu hajawahi kusitisha mazungumzo Yake na mwanadamu; Yeye hajawahi kujificha kutoka kwa binadamu, wala Yeye hajajificha. Fikira Zake, mawazo Yake, maneno Yake na matendo Yake vyote vimefichuliwa kwa mwanadamu. Kwa hivyo, mradi tu mwanadamu angependa kumjua Mungu, anaweza kumwelewa hatimaye na kumjua Yeye kupitia aina zote za mambo na mbinu. Sababu inayomfanya binadamu kufikiria kwa kutojua kwamba Mungu amemwepuka kimakusudi, kwamba Mungu amejificha kimakusudi kutoka kwa binadamu, kwamba Mungu hana nia yoyote ya kumruhusu mwanadamu kuelewa na kumjua Yeye, ni kwamba hajui Mungu ni nani, wala asingependa kujua Mungu; na hata zaidi, hajali kuhusu fikira, matamshi au matendo ya Muumba.... Kusema kweli, kama mtu atatumia tu muda wake wa ziada vizuri katika kuzingatia na kuelewa matamshi au matendo ya Muumba na kuuweka umakinifu mchache kwa fikira za Muumba na sauti ya moyo Wake, haitakuwa vigumu kwa wao kutambua ya kwamba fikira, maneno na matendo ya Muumba, vyote vinaonekana na viko wazi. Vilevile, itachukua jitihada kidogo kutambua kwamba Muumba yuko miongoni mwa binadamu siku zote, kwamba siku zote Anazungumza na binadamu na uumbaji mzima, na kwamba Anatekeleza matendo mapya, kila siku. Hali Yake halisi na tabia vyote vimeelezewa katika mazungumzo Yake na binadamu; fikira na mawazo Yake vyote vinafichuliwa kabisa kwenye matendo Yake haya; Anaandamana na kufuatilia mwanadamu siku zote. Anaongea kimyakimya kwa mwanadamu na uumbaji wote kwa maneno Yake ya kimyakimya: Mimi niko juu ya ulimwengu, na Mimi nimo miongoni mwa uumbaji Wangu. Ninawaangalia, Ninawasubiri; Niko kando yenu.... Mikono yake ni yenye joto na thabiti; nyayo Zake ni nuru; sauti Yake ni laini na yenye neema, umbo Lake linapita na kugeuka, linakumbatia binadamu wote; uso Wake ni mzuri na mtulivu. Hajawahi kuondoka, wala Hajatoweka. Usiku na mchana, Yeye ndiye rafiki wa karibu na wa siku zote wa mwanadamu, ashiyemwacha kamwe. Utunzaji wake wa kujitolea na huba maalum kwa binadamu, pamoja na kujali Kwake kwa kweli na upendo kwa binadamu, vyote vilionyeshwa kwa utaratibu wakati Alipokuwa akiuokoa mji wa Ninawi. Haswa, mabadilishano ya mazungumzo kati ya Yehova Mungu na Yona yaliweza kuweka msingi wa huruma ya Muumba kwa mwanadamu ambaye Yeye Mwenyewe Aliumba. Kupitia kwa maneno haya, unaweza kupata ufahamu wa kina wa hisia za dhati za Mungu kwa binadamu ...

Kifungu kifuatacho kimerekodiwa kwenye kitabu cha Yona 4:10-11: “Kisha Yehova akasema, Umeuonea mtango huruma, ambao hujafanyia kazi, wala kuukuza; ambao ulimea kwa usiku mmoja, na kufa kwa usiku mmoja: Nami sipaswi kuonea Ninawi huruma, mji ule mkuu, ulio na zaidi ya watu elfu mia na ishirini ndani yake ambao hawawezi kutambua kati ya mkono wao wa kulia na mkono wao wa kushoto; na pia mifugo wengi?” Haya ni maneno halisi ya Yehova Mungu, mazungumzo kati Yake na Yona. Huku mabadilishano ya mazungumzo haya

yakiwa mafupi, yamejaa utunzaji wa Muumba kwa mwanadamu na kutotaka Kwake kukata tamaa. Matamshi haya yanaonyesha mtazamo na hisia za kweli ambazo Mungu anashikilia ndani ya moyo Wake kuhusu uumbaji Wake, na kupitia kwa maneno haya yaliyowekwa wazi, ambayo yanasikizwa kwa nadra sana na binadamu, Mungu anakariri nia Zake za kweli kwa binadamu. Mabadilishano ya mazungumzo haya yanawakilisha mtazamo ambao Mungu alishikilia kwa watu wa Ninawi—lakini mtazamo aina hii ni upi? Ni mtazamo Alioshikilia kuhusu watu wa Ninawi kabla na baada ya kutubu kwao. Mungu huchukulia binadamu kwa njia sawa. Ndani ya maneno haya mtu anaweza kupata fikira Zake, pamoja na tabia Yake.

Je, ni fikira zipi za Mungu zinafichuliwa katika maneno haya? Usomaji wa makini unafichua mara moja kwamba Anatumia neno “huruma”; matumizi ya neno hili yanaonyesha mtazamo wa kweli wa Mungu kwa binadamu.

Kwa kiwango cha maana ya juu juu, watu wanaweza kufasiri neno “huruma” kwa njia tofauti: Kwanza, inamaanisha “kupenda na kulinda, kuhisi huruma kuhusu kitu fulani”; pili, inamaanisha “kupenda kwa dhati”; na hatimaye, inamaanisha “kutokuwa radhi kukiumiza kitu fulani na kutoweza kuvumilia kufanya hivyo.” Kwa ufupi, unaashiria yale mahaba na upendo wa dhati, pamoja na kutokuwa radhi kukata tamaa na kumwacha mtu au kitu; unamaanisha huruma ya Mungu na uvumilivu kwa mwanadamu. Ingawaje Mungu alitumia neno linalotamkwa mara nyingi miongoni mwa binadamu, matumizi ya neno hili yanaweka wazi sauti ya moyo wa Mungu na mtazamo Wake kwa mwanadamu.

Huku mji wa Ninawi ukiwa umejaa watu waliopotoka, walio waovu, na wenye udhalimu kama wale wa Sodoma, kutubu kwao kulisababisha Mungu kubadilisha moyo Wake na kuamua kutowaangamiza. Kwa sababu mwitikio wao kwa maneno na maagizo ya Mungu ulionyesha mtazamo uliokuwa na tofauti kavu na ule wa wananchi wa Sodoma, na kwa sababu ya utiifu wao wa dhati kwa Mungu na kutubu kwa uaminifu dhambi zao, pamoja na tabia yao ya kweli na dhati kwa hali zote, Mungu kwa mara nyingine alionyesha huruma Yake ya moyoni naye akaweza kuwapa. Tuzo ya Mungu na huruma Yake kwa binadamu haiwezekani kwa yeyote yule kurudufu; hakuna mtu anayeweza kumiliki huruma au uvumilivu wa Mungu, wala hisia Zake za dhati kwa binadamu. Je, yupo yeyote unayemwona kuwa mwanamume au mwanamke mkuu, au hata mwanamume mkuu zaidi, ambaye angeweza, kutoka katika mtazamo mkuu, akiongea kama mwanamume au mwanamke mkuu au kwenye sehemu ya mamlaka ya juu, kutoa aina hii ya kauli kwa mwanadamu au viumbe? Ni nani miongoni mwa wanadamu anayeweza kujua hali za maisha ya binadamu kama viganja vya mkono wake? Ni nani anayeweza kuvumilia mzigo na jukumu la kuwepo kwa binadamu? Nani aliye na sifa ya kutangaza kuangamizwa kwa mji? Na ni nani aliye na sifa ya kuusamehe mji? Ni nani wanaoweza kusema wanafurahia uumbaji wao

binafsi? Muumba Pekee! Muumba pekee ndiye aliye na upole kwa wanadamu hawa. Muumba pekee ndiye anayeonyesha mwanadamu huyu rehema na huba. Muumba pekee ndiye anayeshikilia huba ya kweli, isiyovunjika kwa mwanadamu huyu. Vilevile, Muumba pekee ndiye anayeweza kumpa huruma mwanadamu huyu na kufurahia viumbe vyake vyote. Moyo wake waruka na kuumia kwa kila matendo ya mwanadamu: Ameghadhibishwa, dhikishwa, na kuhuzunishwa juu ya maovu na kupotoka kwa binadamu; Ameshukuru, amefurahia, amekuwa mwenye kusamehe na mwenye kushangilia kutokana na kutubu na kuamini kwa binadamu; kila mojawapo ya fikira na mawazo Yake vyote yapo juu ya na yanazungukia mwanadamu; kile Alichio na anacho vyote vinaonyeshwa kwa uzima au kwa minajili ya mwanadamu; uzima wa hisia Zake vyote vimeingiliana na uwepo wa mwanadamu. Kwa minajili ya mwanadamu, Anasafiri na kuzungukazunguka; kwa utaratibu Anatoa kila sehemu ya maisha Yake; Anajitolea kila dakika na sekunde ya maisha Yake.... Hajawahi kujua namna ya kuyahurumia maisha Yake, ilhali siku zote Amehurumia na kufurahia mwanadamu ambaye Yeye Mwenyewe aliumba.... Anatoa kila kitu Alichonacho kwa binadamu huu.... Yeye anatoa huruma na uvumilivu Wake bila masharti na bila matarajio ya kufidiwa. Anafanya hivi tu ili mwanadamu aweze kuendelea kuwepo mbele ya macho Yake, kupokea toleo Lake la maisha; Anafanya hivi tu ili mwanadamu siku moja aweze kunyenyekea mbele Yake na kutambua kwamba Yeye ni yule anayetosheleza kuwepo kwa binadamu na kuruzuku maisha ya viumbe vyote.

Muumba Aonyesha Hisia Zake za Kweli Kwa Binadamu

Mazungumzo haya kati ya Yehova Mungu na Yona bila shaka ni onyesho la hisia za kweli za Muumba juu ya binadamu. Kwa upande mmoja yanafahamisha watu kuhusu ufahamu wa Muumba wa asili yote yaliyo katika ukuu Wake; kama vile Yehova Mungu alivyosema, “Nami sipaswi kuonea Ninawi huruma, mji ule mkuu, ulio na zaidi ya watu elfu mia na ishirini ndani yake ambao hawawezi kutambua kati ya mkono wao wa kulia na mkono wao wa kushoto; na pia mifugo wengi?” Kwa maneno mengine, ufahamu wa Ninawi na Mungu haukuwa hata karibu na wa laana. Hakujua tu idadi ya viumbe vilivyo hai ndani ya mji (wakiwemo watu na mifugo), bali Alijua pia ni wangapi wasingeweza kutambua kati ya mikono yao ya kulia na kushoto—yaani, ni watoto na vijana wangapi walikuwepo. Hii ni ithibati thabiti ya ufahamu bora kuhusu mwanadamu. Kwa upande mwingine mazungumzo haya yanafahamisha watu kuhusu mtazamo wa Muumba kwa binadamu, ambako ni kusema kwamba uzito wa binadamu katika moyo wa Muumba. Ni vile tu Yehova Mungu alivyosema: “Umeuonea mtango huruma, ambao hujafanyia kazi, wala kuukuza; ambao ulimea kwa usiku mmoja, na kufa kwa usiku mmoja: Nami sipaswi kuonea Ninawi huruma, mji ule mkuu...?” Haya ndiyo maneno ya Yehova Mungu kuhusu lawama kwa Yona lakini yote ni kweli.

Ingawaje Yona alikuwa ameaminiwa kutangaza matamshi ya Yehova Mungu kwa watu wa Ninawi, hakuelewa nia za Yehova Mungu, wala hakuelewa wasiwasi na matarajio Yake kwa watu wa mji huu. Kupitia kwa kemeo hili Mungu alinua kumwambia kwamba binadamu ulikuwa zao la mikono Yake mwenyewe, na kwamba Mungu alikuwa ametia jitihada za dhati kwa kila mtu; kila mtu alisheheni matumaini ya Mungu; kila mtu alifurahia ruzuku ya maisha ya Mungu; kwa kila mtu, Mungu alikuwa amelipia gharama ya dhati. Kemeo hili lilimfahamisha Yona kwamba Mungu aliufurahia binadamu, kazi ya mikono Yake mwenyewe, kama vile tu ambavyo Yona mwenyewe aliufurahia mtango. Mungu kwa vyovyote vile asingewaacha kwa urahisi kabla ya ule muda wa mwisho unaowezekana; vilevile, kulikuwa na watoto wengi na mifugo isiyo na hatia ndani ya mji. Wakati wa kushughulikia mazao haya machanga na yasiyojua uumbaji wa Mungu, ambayo yasingeweza hata kutofautisha mikono yao ya kulia na ile ya kushoto, Mungu hakuweza kamwe kukomesha maisha yao na kuamua matokeo yao kwa njia ya haraka hivyo. Mungu alitumai kuwaona wakikua; Alitumai kwamba wasingetembea njia ile ile kama wakubwa wao, kwamba wasingeweza kusikia tena onyo la Yehova Mungu, na kwamba wangeshuhudia mambo ya kale ya Ninawi. Na hata zaidi Mungu alitumai kuiona Ninawi baada ya kuweza kutubu, kuuona mustakabali wa Ninawi kufuatia kutubu kwake, na muhimu zaidi, kuiona Ninawi ikiishi katika huruma za Mungu kwa mara nyingine tena. Kwa hivyo, kwa macho ya Mungu, yale mazao ya uumbaji wake ambayo hayangeweza kutofautisha mikono yao ya kulia na kushoto yalikuwa mustakabali wa Ninawi. Wangeweza kubeba na kusimulia hadithi ya kale iliyostahili dharau, kama vile tu ambavyo wangeweza kusimulia wajibu muhimu wa kushuhudia hadithi ya kale ya Ninawi na mustakabali wake kupitia kwa mwongozo wa Yehova Mungu. Katika tangazo hili la hisia Zake za kweli, Yehova Mungu aliwasilisha huruma ya Muumba kuhusu binadamu kwa uzima wake. Lilionyesha binadamu kwamba “ile huruma ya Muumba” si kauli tupu tu, wala si ahadi isiyotimizika; ilikuwa na kanuni, mbinu na majukumu ya kimsingi. Yeye ni kweli na halisi, na hatumii uwongo au utapeli wowote, na kwa njia ii hii huruma Yake inawekewa binadamu katika kila wakati na enzi. Hata hivyo, hadi siku hii, mabadilishano ya mazungumzo ya Muumba na Yona ndiyo kauli moja, na ya kipekee ya matamshi yanayoelezea ni kwa nini Anaonyesha huruma kwa binadamu, jinsi Anavyoonyesha huruma kwa binadamu, ni vipi Alivyo na uvumilivu kwa binadamu na hisia Zake za kweli kuhusu binadamu. Mazungumzo haya ya Yehova Mungu yenye uchache na uwazi yanaonyesha fikira Zake kamili kuhusu binadamu; ni maonyesho ya ukweli ya mtazamo wa moyo Wake kwa binadamu, na ni ushahidi thabiti wa kutoa Kwake kwingi kwa huruma juu ya binadamu. Huruma yake haipewi tu vizazi vya wazee wa binadamu; lakini pia imepewa wanachama wachanga zaidi wa binadamu, kama vile tu ambavyo imekuwa, kuanzia kizazi kimoja hadi kingine. Ingawaje hasira ya Mungu hushushwa mara kwa mara kwenye pembe fulani na enzi fulani za binadamu, huruma ya Mungu haijawahi kusita. Kupitia kwa huruma Yake, Yeye huongoza na kuelekeza kizazi kimoja cha

uumbaji Wake hadi kingine, huruzuku na kukifaa kizazi kimoja cha uumbaji hadi kingine, kwa sababu hisia Zake za kweli kwa binadamu hazitawahi kubadilika. Vile tu Yehova Mungu alivyosema: “Nami sipaswi kuonea Ninawi huruma...?” Siku zote amefurahia uumbaji Wake mwenyewe. Hii ndiyo huruma ya tabia ya haki ya Muumba, na ndio pia upekee usio na kasoro wa Muumba!

Aina Tano za Watu

Kwa sasa, Nitaacha ushirika wetu kuhusu tabia ya haki ya Mungu umalizikie hapo. Kinachofuata Nitaainisha wafuasi wa Mungu katika kategoria mbalimbali, kulingana na ufahamu wao wa Mungu na ufahamu wao na kile wamepitia kuhusiana na tabia ya haki Yake, ili muweze kujua awamu ambayo kwa sasa mnapatikana ndani pamoja na kimo chenu cha sasa. Kuhusiana na maarifa yao ya Mungu na ufahamu wao wa tabia Yake ya haki, awamu na kimo tofauti ambavyo watu huwa navyo vinaweza kugawanywa katika aina tano. Mada hii imeelezewa kwa msingi wa kumjua Mungu wa kipekee na tabia Yake ya haki; kwa hivyo, unaposoma maudhui yafuatayo, unafaa kujaribu kwa makini kuchambua ni kiwango kipi haswa cha ufahamu na maarifa ulichonacho kuhusiana na upekee wa Mungu na tabia Yake ya haki, na kisha utumie hayo kujua ni awamu gani ambayo kwa kweli unapatikana ndani, kimo chako ni kikubwa vipi kwa kweli, na wewe ni aina gani ya mtu kwa kweli.

Aina ya Kwanza: Hatua ya Mtoto Mchanga aliyefungwa kwa Vitambaa

Mtoto mchanga aliyefungwa kwa vitambaa ni nini? Mtoto mchanga aliyefungwa kwa vitambaa ni mtoto mchanga ambaye ndio mwanzo ameingia kwenye ulimwengu huu, amezaliwa. Huu ndio wakati ambao watu wako katika awamu ndogo zaidi na isiyo na ukomavu.

Watu katika awamu hii kimsingi hawamiliki utambuzi au ufahamu wowote wa masuala ya kuamini Mungu. Wamekanganywa na hawajui kila kitu. Watu hawa huenda wamemsadiki Mungu kwa muda mrefu au kwa muda usiokuwa mrefu, lakini hali yao ya kukanganywa na kutojua kimo chao halisi kinawaweka kwenye awamu ya mtoto mchanga aliyefungwa kwa vitambaa. Ufafanuzi wa hakika wa hali hii ya mtoto mchanga aliyefungwa kwa vitambaa ni kama vile: Haijalishi ni muda upi ambao aina hii ya mtu amesadiki Mungu, siku zote atakuwa mpumbavu, atachanganyikiwa na ataonyesha werevu au uamuzi wa kiwango kidogo sana; hajui ni kwa nini anasadiki Mungu, wala hajui Mungu ni nani au Mungu ni nini. Ingawaje anafuata Mungu, hakuna ufafanuzi halisi wa Mungu katika moyo wake, na hawezi kuamua kama yule anayemfuata ni Mungu, sikuambii hata kama kweli anafaa kumsadiki Mungu na kumfuata Yeye. Hizi ndizo hali za kweli za aina hii ya mtu. Fikira za watu hawa zimezingirwa na ukungu, na kama nitasema wazi, imani yao ni ile ya mkanganyo. Siku zote wanakuwa katika hali ya

mkanganyiko na utupu; kuwa mpumbavu, kuchanganyikiwa na kuonyesha werevu au uamuzi wa kiwango kidogo sana ndivyo vitu vinavyofanya muhtasari wa hali zao. Hawajawahi kuona wala kuhisi uwepo wa Mungu, na hivyo basi, kuwazungumzia kuhusu kujua Mungu ni sawa tu na kuwafanya kusoma kitabu kilichoandikwa kwa maandiko ya hieroglifu maandiko au ishara zisizofahamika; hawataelewa wala kuyakubali. Kwao, kujua Mungu ni sawa na kusikia kisa cha kifantasia. Huku fikira zao zikiwa zinaweza kuwa na ukungu, kwa hakika wanasadiki kwa dhati kwamba kujua Mungu ni kupoteza muda na jitihada. Huyu ndiye mtu wa aina ya kwanza: mtoto mchanga aliyefungwa kwa vitambaa.

Aina ya Pili: Hatua ya Mtoto Mchanga Anayenyonya

Akilinganishwa na mtoto mchanga aliyefungiwa ndani ya vitambaa, aina hii ya mtu amepiga hatua fulani. Kwa bahati mbaya, bado hawana ufahamu wa Mungu kamwe. Wangali wanakosa ufahamu wazi wa na utambuzi wa Mungu, na hawaelewi vizuri sana ni kwa nini wanafaa kumsadiki Mungu, lakini katika mioyo yao wanalo kusudi lao binafsi na mawazo wazi. Hawajihusishi na suala la kama ni sahihi kumsadiki Mungu. Lengo na kusudi wanalotafuta kupitia kwa imani ya Mungu ni kufurahia neema Yake, kuwa na furaha na amani, kuishi maisha yenye utulivu, kuwa na utunzaji na ulinzi wa Mungu na kuishi katika baraka za Mungu. Hawajali kiwango ambacho wanamjua Mungu; hawana msisimko wa kutafuta kuelewa Mungu, wala hawashughuliki na kile ambacho Mungu anafanya au kile ambacho Angependa kufanya. Wanatafuta tu bila mwelekeo kufurahia neema Yake na kupata baraka Zake nyingi; wanatafuta kupokea baraka mara mia moja kwenye umri wa sasa, na maisha ya baadaye kwenye miaka ijayo. Fikira zao, matumizi na kujitolea kwao, pamoja na kuteseka kwao, vyote vinalo lengo moja: kupokea neema na baraka za Mungu. Hawana shughuli na kitu kingine chochote. Aina hii ya mtu bila shaka ana hakika kwamba Mungu anaweza kuwalinda wakawa salama na kuwapa neema Yake. Mtu anaweza kusema kwamba hawana kivutio chochote katika na hawana mwelekeo sana kuhusiana na kwa nini Mungu angependa kumwokoza binadamu au matokeo ambayo Mungu angependa kupata kutokana na matamshi na kazi Yake. Hawajawahi kutia jitihada za kujua hali halisi ya Mungu na tabia ya haki, wala hawawezi kujipa moyo na kuwa na nia ya kufanya hivyo. Hawahisi kumakinikia katika mambo haya, wala hawapendi kuyajua. Hawapendi hata kuulizia kuhusu kazi ya Mungu, mahitaji ya Mungu kwa binadamu, mapenzi ya Mungu au kitu chochote kingine kinachohusiana na Mungu; wala hawawezi kuwa na msukumo wa kuulizia mambo haya. Hii ni kwa sababu wanasadiki masuala haya hayahusiani na kufurahia kwao kwa neema ya Mungu; wanajali tu Mungu anayeweza kuwapa neema na ambaye ana uhusiano na masilahi yao ya kibinafsi. Hawana haja kamwe na kitu kingine chochote, na kwa hivyo hawawezi kuingia kwenye uhalisi wa ukweli, licha ya miaka mingapi ambayo wamemsadiki Mungu. Bila kuwepo yeyote wa kuwafunza neno la Bwana, mara nyingi ni

vigumu kwao kuendelea kupiga hatua katika njia ya imani ya Mungu. Kama hawawezi kufurahia furaha yao na amani ya awali au kufurahia neema ya Mungu, basi wana uwezekano mkubwa wa kujiondoa. Huyu ndiye mtu wa aina ya pili: mtu anayekuwepo kwenye awamu ya mtoto mchanga wa kunyonya.

Aina ya Tatu: Hatua ya Mtoto Mchanga Anayeachishwa Ziwa, au Hatua ya Mtoto Mdogo

Kundi hili la watu humiliki ufahamu fulani wenye uwazi. Watu hawa wanao ufahamu kwamba kufurahia neema ya Mungu hakumaanishi kwamba wao wenyewe wanamiliki uzoefu wa kweli; wanao ufahamu kwamba wasipochoka katika kutafuta furaha na amani, katika kutafuta neema, au kama wanaweza kushuhudia kwa kujadiliana yale yote ambayo wamepitia katika kufurahikia kwao kwa neema ya Mungu au kwa kumsifu Mungu kwa baraka Zake ambazo amewapa, mambo haya hayamaanishi kwamba wanayo maisha, wala hayamaanishi kwamba wanao uhalisi wa ukweli. Tukianza katika fahamu yao, wanasita kufurahia matumaini yasiyo na mipaka kwamba wataandamana tu na neema ya Mungu; badala yake, wakati wanapofurahia neema ya Mungu, wanapenda wakati uo huo kufanya kitu kwa ajili ya Mungu; wako radhi kutekeleza wajibu wao, kuvumilia ugumu kidogo na uchovu, kuwa na kiasi fulani cha ushirikiano na Mungu. Hata hivyo, kwa sababu kufuatilia kwao katika imani yao katika Mungu kumetiwa najisi sana, kwa sababu nia za kibinafsi na matamania waliyo nayo ni makali mno, kwa sababu tabia yao ni yenye kiburi kisicho na mipaka, ni vigumu sana kwao kutosheleza tamania la Mungu au kuwa watiifu kwa Mungu; hivyo basi, wao mara nyingi hawawezi kutambua matamania yao ya kibinafsi au kuheshimu ahadi zao kwa Mungu. Mara nyingi wanajipata katika hali za kukinzana: Wanapenda sana kutosheleza Mungu hadi kwenye kiwango kikubwa zaidi kinachowezekana, ilhali wanatumia uwezo wao wote kumpinga Yeye; mara nyingi wanaweka nadhiri kwa Mungu lakini kwa haraka sana wanaishia kukwepa nadhiri zao. Hata mara nyingi wanajipata katika hali nyingine kinzani: Wanasadiki kwa dhati katika Mungu ilhali wanamkataa Mungu na kila kitu kinachotokana na Yeye; wanatumai kwa hamu kwamba Mungu atawapa nuru, atawaongoza, atawaruzuku na kuwasaidia, ilhali bado wanatafuta njia yao wenyewe. Wanapenda kuelewa na kujua Mungu, ilhali hawako radhi kuwa na uhusiano wa karibu na Yeye. Badala yake, siku zote wanamwepuka Mungu; mioyo yao haiko wazi kumkaribisha. Huku wakiwa na ufahamu wa juujuu na uzoefu wa maana ya moja kwa moja ya matamshi ya Mungu na ya ukweli, na dhana ya juujuu ya Mungu na ukweli, katika akili iliyofichika bado hawawezi kuthibitisha au kuamua kama Mungu ni ukweli; hawawezi kuthibitisha kama Mungu ni wa haki kwa kweli; wala hawawezi kuamua ule uhalisi wa tabia ya Mungu na hali halisi, sikuambii hata uwepo Wake wa kweli. Imani yao katika Mungu siku zote ina shaka na kutoelewana kwingi, na pia kunazo fikira za maono na dhana mbalimbali. Wanapofurahia neema ya Mungu, wanapitia pia bila kutaka au wanatenda baadhi ya kile

wanachosadiki kuwa ukweli unaowezekana, ili kunufaisha imani yao, kukuza kile ambacho wamepitia katika kusadiki Mungu, kuthibitisha ufahamu wao wa kusadiki Mungu, na kutosheleza majisifu yao ya kutembelea njia ya maisha ambayo wao wenyewe wameanzisha na kukamilisha mkondo wa haki wa mwanadamu. Wakati uo huo wanafanya pia mambo haya ili kutosheleza tamanio lao binafsi la kufaidi baraka, ili wawekeane dau ndio waweze kupata baraka kubwa zaidi za binadamu, ili kutimiza maazimio ya maono na matamania ya kimaisha ya kutopumzika mpaka pale ambapo wamefaidi Mungu. Watu hawa kwa nadra sana wanaweza kupokea nuru ya Mungu, kwani tamanio lao na nia yao ya kufaidi baraka ni muhimu sana kwao. Hawana tamanio la na hawawezi kuvumilia kutupilia mbali hili. Wanaogopa kwamba bila ya tamanio la kufaidi baraka, bila ya maono waliyotamani kwa muda mrefu ya kutopumzika mpaka pale ambapo wamefaidi Mungu, wataweza kukosa motisha ya kusadiki Mungu. Kwa hivyo, hawapendi kukabiliana na uhalisi. Hawapendi kukabiliana na matamshi ya Mungu au kazi ya Mungu. Hawapendi kukabiliana na tabia au hali halisi ya Mungu, sikuambii hata kuzungumzia mada ya kumjua Mungu. Hii ni kwa sababu mara tu Mungu, hali Yake halisi na tabia Yake ya haki vinapobadilisha maono yao, ndoto zao zitatoweka hivyo bila kuonekana; imani yao inayodhaniwa kuwa safi na “sifa njema” zilizokusanywa baada ya miaka ya kazi ngumu zitatoweka zote na kutokuwa na manufaa yoyote; “eneo” lao ambalo wameshinda kupitia kwa jasho na damu yao kwa miaka na mikaka itakuwa karibu kusambaratika. Hii itamaanisha kwamba miaka yao mingi ya kazi ya sulubu na jitihada vyote vimekuwa bure bilashi, kwamba lazima waanze tena kutoka sehemu ya kutokuwa na chochote. Haya ndiyo maumivu magumu zaidi kwao kuvumilia katika mioyo yao, na ni matokeo ambayo wanatamani kwa kiasi cha chini zaidi kuona; hivyo basi siku zote wamefungwa katika aina hii ya kutosonga mbele, na kukataa kurudi nyuma. Huyu ndiye mtu wa aina ya tatu: mtu anayekuwa katika awamu hii ya mtoto mchanga wa kuachishwa ziwa.

Aina tatu za watu waliofafanuliwa hapo juu—kwa maneno mengine, watu wanaopatikana katika awamu hizi tatu—hawamiliki imani yoyote ya kweli katika utambulisho na hadhi ya Mungu au katika tabia Yake halisi, wala hawana utambuzi wowote wazi, wa hakika au thibitisho la mambo haya. Kwa hivyo, ni vigumu sana kwa aina hizi tatu za watu kuingia kwenye uhalisi wa ukweli, na ni vigumu pia kwa wao kupokea huruma, nuru au mwangaza wa Mungu kwa sababu ya namna ambavyo wanasadiki Mungu na mtazamo wao wa kimakosa kwa Mungu unamfanya Yeye kutoweza kutekeleza kazi yoyote ndani ya mioyo yao. Shaka zao, kuelewa kwao vibaya na kufikiria kwao kuhusiana na Mungu kumezidi imani yao na maarifa ya Mungu. Hizi ni aina tatu za watu walio katika hatari kubwa, na ni hatua tatu hatari sana. Wakati mtu anapoendeleza mtazamo wa shaka kwa Mungu, hali halisi ya Mungu, utambulisho wa Mungu, lile suala la kama Mungu ni ukweli na uhalisi wa uwepo Wake na kwamba hawezi kuwa na

hakika katika mambo haya, ni vipi ambavyo mtu anaweza kukubali kila kitu kinachotoka kwa Mungu? Mtu anawezaje kukubali hoja kwamba Mungu ni ukweli, njia na uzima? Mtu anawezaje kukubali kuadibu na hukumu ya Mungu? Mtu anawezaje kukubali wokovu wa Mungu? Ni vipi ambavyo aina hii ya mtu anaweza kupokea mwongozo na ruzuku ya kweli kutoka kwa Mungu? Wale ambao wanapatikana katika awamu hizi tatu wanaweza kumpinga Mungu, kupitisha hukumu kwa Mungu, kukufuru Mungu au kusaliti Mungu wakati wowote. Wanaweza kuacha njia ya kweli na kumtoroka Mungu wakati wowote. Mtu anaweza kusema kwamba watu katika awamu hizi tatu wapo katika kipindi hatari sana, kwani hawajaingia kwenye njia sahihi ya kumsadiki Mungu.

Aina ya Nne: Hatua ya Mtoto Anayekomaa, au Kipindi cha Utoto

Baada ya mtu kuachishwa ziwa—yaani, baada ya wao kufurahia kiwango tosha cha neema, mtu anaanza kuchunguza ni nini maana ya kusadiki Mungu, kutaka kuelewa maswali tofauti, kama vile kwa nini binadamu anaishi, binadamu anafaa kuishi vipi, na kwa nini Mungu hutekeleza kazi Yake kwa binadamu. Wakati ambapo mawazo haya yasiyo wazi na mawazo yaliyokanganyikiwa hujitokeza ndani yao, na kuwepo ndani yao, wanaendelea kupokea kunyunyizwa, na wao wanaweza pia kutekeleza wajibu wao. Kwenye kipindi hiki, hawana tena shaka kuhusiana na ukweli wa uwepo wa Mungu, na wanao ung'amuzi sahihi wa ni nini maana ya kumwamini Mungu. Kwenye msingi huu wao hupata maarifa ya utaratibu kuhusu Mungu, na wanapokea kwa utaratibu baadhi ya majibu ya mawazo yao yasiyo wazi na mawazo yaliyokanganyika kuhusiana na tabia ya Mungu na hali halisi. Kwa mujibu wa mabadiliko yao katika tabia yao pamoja na maarifa yao kuhusu Mungu, watu katika awamu hii huanza kushika njia sahihi na kuingia kwenye kipindi cha mpito. Ni katika awamu hii ambapo watu huanza kuwa na maisha. Vionyeshi wazi vya kumiliki maisha ni uamuzi wa taratibu wa maswali mbalimbali yanayohusiana na kumjua Mungu ambayo watu wanakuwa nayo katika mioyo yao—kutoelewana, mawazo, fikira, na ufafanuzi usio wazi wa Mungu—na si kwamba wao huja kusadiki na kujua uhalisi wa uwepo wa Mungu, lakini pia wao huja kumiliki ufasili wazi wa Mungu na kuwa na nafasi sahihi ya Mungu katika mioyo yao, na kumfuata Mungu kwa kweli kutabadilisha imani yao isiyo dhahiri. Kwenye awamu hii, watu kwa utaratibu wanaanza kujua kutoelewa kwao katika masuala ya Mungu na kutafuta kwao kimakosa na njia za imani. Wanaanza kutamani ukweli, kutamani kupitia hukumu ya Mungu, kurudiwa na nidhamu, kutamani mabadiliko katika tabia yao. Kwa utaratibu wanaanza kuacha aina zote za dhana na fikira kuhusu Mungu kwenye awamu hii; wakati uo huo wanabadilisha na kurekebisha maarifa yasiyo sahihi kuhusu Mungu na kupata baadhi ya maarifa muhimu na sahihi kuhusu Mungu. Ingawaje sehemu ya maarifa inayomilikiwa na watu katika awamu hii si mahususi au sahihi sana, kwa kiwango cha chini zaidi wanaanza kwa utaratibu kuacha dhana zao, maarifa ya

kimakosa na kutoelewa mambo kuhusu Mungu; hawaendelezi tena dhana zao binafsi na fikira zao kuhusu Mungu. Wanaanza kujifunza namna ya kuacha—kuacha mambo yanayopatikana miongoni mwa dhana zao binafsi, kutoka kwa maarifa yao na kutoka kwa Shetani; wanaanza kuwa radhi kutii mambo sahihi na mazuri, hata kwa mambo yanayotoka kwenye matamshi ya Mungu na kutii ukweli. Wanaanza pia kujaribu kupitia matamshi ya Mungu, kujua kibinafsi na kutekeleza matamshi Yake, kukubali matamshi Yake kama kanuni za hatua zao na kama msingi wa kubadilisha tabia yao. Kwenye kipindi hiki, watu bila kufahamu wanaikubali hukumu na kuadibu kwa Mungu, wanakubali bila fahamu matamshi ya Mungu kuwa maisha yao. Huku wakikubali hukumu, kuadibu kwa Mungu, na kukubali matamshi ya Mungu, wanaendelea kuwa na ongezeko la kufahamu na wanaweza kuhisi kwamba Mungu wanayemsadiki ndani ya mioyo yao kweli yupo. Kwa maneno ya Mungu, hali yao wanayopitia na maisha yao, wanazidi kuhisi kwamba Mungu siku zote amesimamia hatima ya binadamu, kumwongoza binadamu na kuruzuku binadamu. Kupitia kwa ushirikiano wao na Mungu, wanaanza kwa utaratibu kuthibitisha uwepo wa Mungu. Kwa hivyo, kabla ya wao kutambua, tayari wameuidhinisha bila kufahamu na kusadiki kwa dhati katika kazi ya Mungu, na wameidhinisha matamshi ya Mungu. Baada ya watu kuidhinisha matamshi ya Mungu, na kuidhinisha kazi ya Mungu, bila kusita wanajikataa, wanakataa dhana zao binafsi, wanakataa maarifa yao binafsi, wanakataa fikira zao binafsi, na wakati uo huo wanatafuta bila kusita ukweli ni nini na mapenzi ya Mungu ni nini. Maarifa ya watu kuhusu Mungu ni ya juujuu sana kwenye kipindi hiki cha maendeleo—hata hawawezi kufafanua wazi maarifa haya kwa kutumia matamshi, wala hawawezi hata kufafanua kimahususi—na wanao ufahamu unaohusu utambuzi; hata hivyo, wakati awamu hii inawekwa sambamba na zile awamu tatu zilizotangulia, maisha ya watu wasiokomaa katika kipindi hiki tayari yameanza kupokea kunyunyizia na ruzuku ya matamshi ya Mungu, na tayari yameanza kuota. Ni sawa na mbegu iliyozikwa ardhini; baada ya kupokea unyevunyevu na virutubisho, lazima itapenyeza kupitia kwenye mchanga; kuota kwake kunawakilisha kuzaliwa kwa maisha mapya. Kuzaliwa huku kwa maisha mapya kunaruhusu mtu kuona vionyeshi vya maisha. Kupitia kwa maisha, watu wataweza kukua. Kwa hivyo, juu ya misingi hii—kwa utaratibu wanaanza kurudi katika njia sahihi ya kusadiki katika Mungu, kuacha dhana zao binafsi, kupata mwongozo wa Mungu—maisha ya watu yataweza kukua bila shaka hatua kwa hatua. Ni katika msingi gani ndipo ukuaji huu unapimwa? Unapimwa kulingana na uzoefu wao na maneno ya Mungu na ufahamu wao wa kweli kuhusu tabia ya haki ya Mungu. Ingawaje wanaona jambo hili likiwa gumu sana katika kutumia maneno yao binafsi ili kufafanua kwa usahihi maarifa yao kuhusu Mungu na hali Yake halisi kwenye kipindi hiki cha ukuaji, kundi hili la watu haliko radhi tena kufuatilia kimsingi furaha kupitia kwa kufurahia neema ya Mungu, au kufuatilia kusudi lao la kusadiki Mungu, ambapo ni kupokea neema Yake. Badala yake, wako radhi kutafuta kuishi kwa neno la Mungu, ili kuwa walengwa wa wokovu wa Mungu. Vilevile, wanamiliki ujasiri na wako

tayari kukubali hukumu na kuadibu kwa Mungu. Hii ndiyo alama ya mtu aliye katika awamu ya kukua.

Ingawaje watu katika awamu hii wanayo maarifa fulani kuhusu tabia ya haki ya Mungu, maarifa yao si dhahiri wala bainifu. Huku wakiwa hawawezi kufafanua wazi hali hii, wanahisi kwamba tayari wamefaidi kitu fulani ndani kwa ndani, kwani wamepata kipimo fulani cha maarifa na ufahamu wa tabia ya haki ya Mungu kupitia kwa kuadibu kwa Mungu na hukumu yake; hata hivyo yote haya ni kana kwamba ni ya juujuu, na bado yangali katika awamu ya kimsingi. Kundi hili la watu linao msimamo wa maoni thabiti kuhusiana na neema ya Mungu. Msimamo huu wa maoni unaelezewa kupitia kwenye mabadiliko ya malengo wanayoyatafuta na njia ambayo wanayatafutia. Tayari wameona—katika maneno na kazi ya Mungu, kwenye aina zote za mahitaji Yake ya binadamu na kwenye ufunuo Wake wa binadamu—kwamba kama bado hawatafuatilia ukweli, kama bado hawatafuti kuingia kwenye uhalisia, kama bado hawatafuti kutosheleza na kujua Mungu huku wakipitia maneno Yake, watapoteza umuhimu katika kusadiki Mungu. Wanaona haijalishi ni kiwango kipi ambacho wanafurahia neema ya Mungu, hawawezi kubadilisha tabia yao, kutosheleza Mungu au kumjua Mungu, na kwamba wakiendelea kuishi miongoni mwa neema ya Mungu, hawatawahi kutimiza ukuaji, kupata uzima au kuweza kupokea wokovu. Kwa muhtasari, kama mtu hawezi kupitia maneno ya Mungu kwa njia ya kweli na hawezi kumjua Mungu kupitia kwa maneno Yake, mtu huyo daima dawamu atabakia katika awamu ile ya mtoto mchanga na hatawahi kupiga hatua yoyote mbele kwenye ukuaji wa maisha yake. Kama daima dawamu utakuwepo kwenye hatua ya mtoto mchanga, kama kamwe huingii kwenye uhalisi wa neno la Mungu, kama kamwe huna neno la Mungu kama maisha yako, kama kamwe huna imani na maarifa ya kweli kuhusu Mungu, je, kuna uwezekano wowote kwako wewe kufanywa kuwa kamili na Mungu? Hivyo basi, yeyote anayeingia katika uhalisi wa neno la Mungu, yeyote anayekubali neno la Mungu kuwa maisha yake, yeyote anayeanza kukubali kuadibu na hukumu ya Mungu, yeyote ambaye tabia yake potovu inaanza kubadilika, na yeyote aliye na moyo unaotamani ukweli, analo tamanio la kumjua Mungu, analo tamanio la kukubali wokovu wa Mungu—watu hawa ndio wale wanaomiliki uzima kwa kweli. Hii kwa kweli ndiyo aina ya nne ya mtu, ile ya mtoto anayekomaa, mtu aliye katika awamu ya utoto.

Aina ya Tano: Hatua ya Maisha Yaliyokomaa, au Hatua ya Mtu Mzima

Baada ya kupitia awamu ya mtoto mchanga hadi ya utoto, awamu hii ya ukuaji uliojaa kupindua kunakojirudia, maisha ya watu tayari yamekuwa thabiti, hatua yao ya kusonga mbele haisiti tena, wala hakuna yeyote anayeweza kuwazuia. Ingawaje njia iliyo mbele ingali na mabonde na misukosuko, si wanyonge tena au wenye woga; hawayumbiyumbi tena huko mbele au kupoteza mwelekeo wao. Misingi yao imekita mizizi kwenye hali halisi ya neno la Mungu.

Mioyo yao imevutwa na heshima na ukubwa wa Mungu. Wanatamani kufuata nyayo za Mungu, kujua hali halisi ya Mungu, kujua Mungu kwa uzima Wake.

Watu katika awamu hii tayari wanajua waziwazi ni nani wanayemsadiki, na wanajua waziwazi kwa nini wanafaa kumsadiki Mungu na maana ya maisha yao husika; wanajua pia waziwazi kwamba kila kitu ambacho Mungu huelezea ndicho ukweli. Kwenye miaka yao mingi ya uzoefu, wametambua kwamba bila ya hukumu na kuadibu kwa Mungu, mtu hatawahi kuweza kutosheleza au kumjua Mungu, wala mtu huyo hataweza kuja mbele ya Mungu. Ndani ya mioyo ya watu hawa husika kunalo tamanio thabiti la kujaribiwa na Mungu, ili kuona tabia ya haki ya Mungu huku wakiendelea kujaribiwa, kufikia upendo safi zaidi, na wakati uo huo kuweza kuelewa na kujua Mungu kwa njia ya kweli zaidi. Wale walio katika awamu hii tayari wameaga kwaheri awamu ya mtoto, awamu ya kufurahia neema ya Mungu na kula mkate na kushiba. Hawaweki tena matumaini mengi katika kumfanya Mungu kuvumilia na kuwaonyesha huruma; badala yake, wanao ujasiri wa kupokea na kutumai kupata kuadibu na hukumu isiyosita ya Mungu, ili kuweza kujitenga na tabia yao potovu na hivyo basi kutosheleza Mungu. Maarifa yao kwa Mungu, kufuatilia kwao au shabaha za mwisho za kufuatilia kwao: mambo haya yote yako wazi kabisa katika mioyo yao. Hivyo basi, watu katika awamu ya mtu mzima tayari wameaga kwaheri kabisa awamu ya imani isiyo dhahiri, kwenye awamu ambayo wanategemea neema kupata wokovu, kwenye awamu ya maisha yasiyo komavu yasiyoweza kustahimili majaribio, hadi kwenye awamu ya kutokuwa bainifu, hadi kwenye awamu ya kuyumbayumba, hadi kwenye awamu ya mara kwa mara kutokuwa na njia ya kufuata, hadi kwenye kipindi kisichokuwa thabiti cha kubadilisha kati ya joto na baridi ya ghafla, na hadi kwenye awamu ambapo mtu anafuata Mungu huku ameyafumba macho yake. Aina hii ya mtu hupokea nuru na mwangaza wa Mungu mara kwa mara, na pia mara kwa mara hujihusisha katika ushirikiano na mawasiliano ya kweli na Mungu. Mtu anaweza kusema kwamba watu wanaoishi katika awamu hii tayari wameng'amua sehemu ya mapenzi ya Mungu; wanaweza kupata kanuni za ukweli katika kila kitu wanachofanya; wanajua namna ya kutosheleza tamanio la Mungu. Isitoshe, wamepata pia njia ya kumjua Mungu na wameanza kuwa na ushuhuda wa maarifa yao kwa Mungu. Kwenye mchakato huu wa ukuaji wa utaratibu, wanao ufahamu wa taratibu na maarifa ya mapenzi ya Mungu, ya mapenzi ya Mungu katika kuumba binadamu, ya mapenzi ya Mungu katika kusimamia binadamu; vilevile, kwa utaratibu wanao ufahamu na maarifa ya tabia ya haki ya Mungu kwa mujibu wa hali halisi. Hakuna dhana ya binadamu au kufikiria kunaweza kubadilisha maarifa haya. Huku mtu hawezi kusema kwamba kwenye awamu ya tano maisha ya mtu yamekomaa kabisa au kumwita mtu huyu mwenye haki au mkamilifu, aina hii ya mtu tayari amechukua hatua ya kuelekea kwenye awamu ya ukomavu katika maisha; mtu huyu tayari anaweza kuja mbele ya Mungu, kusimama ana kwa ana na neno la Mungu na kuwa ana kwa ana

na Mungu. Kwa sababu mtu wa aina hii tayari amepitia mengi sana yanayohusu neno la Mungu, amepitia majaribio yasiyokadirika na kupitia matukio yasiyokadirika ya nidhamu, hukumu na kuadibu kutoka kwa Mungu, unyenyekevu wake kwa Mungu si wa kutegemea chochote bali ni kamili. Maarifa yao kwa Mungu yamebadilika kutoka kwenye kufichika akilini hadi kwa maarifa wazi na hakika, kutoka kwenye hali ya juujuu hadi kina, kutoka kwenye hali ya kutoeleweka na kutokuwa bainifu hadi hali ya umakinifu na uyakinifu, na wamebadilika kutoka kwenye kutafutatafuta kwa bidii na kutafuta kwa njia iliyo baridi hadi katika hali ya kuwa na maarifa kwa hakika na utoaji ushuhuda wenye mnato. Inaweza kusemekana kwamba watu katika awamu hii wamemiliki uhalisi wa ukweli wa neno la Mungu, kwamba wamepitia kwenye njia ya utimilifu kama vile Petro alivyopita. Huyu ndiye mtu wa aina ya tano, yule anayeishi katika hali ya kuwa mkomavu—awamu ya kuwa mtu mzima.

Desemba 14, 2013

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee III

Mamlaka ya Mungu (II)

Leo tutaendelea na ushirika wetu kuhusu mada ya “Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee.” Tayari tumekuwa na ushirika mara mbili katika mada hii, wa kwanza kuhusiana na mamlaka ya Mungu na wa pili kuhusiana na tabia ya haki ya Mungu. Baada ya kusikiliza ushirika huu mara mbili, je, mmepata ufahamu mpya wa utambulisho wa Mungu, hadhi, na hali halisi? Je, maono haya yamewasaidia kufikia maarifa mazito zaidi na uhakika wa ukweli kuuhusu uwepo wa Mungu? Leo Ninapanga kufafanua mada hii ya “Mamlaka ya Mungu.”

Kuelewa Mamlaka ya Mungu Kutoka kwa Mitazamo Mikubwa na Midogo

Mamlaka ya Mungu ni ya kipekee. Ndiyo maonyesho ya sifa ya, na hali halisi maalum ya, utambulisho wa Mungu Mwenyewe. Hakuna kiumbe ambacho kiliumbwa wala kile ambacho hakikuumbwa kinachomiliki maonyesho ya sifa kama hizi na hali halisi maalum; Muumba tu ndiye anayemiliki aina hii ya mamlaka. Hivyo ni kusema kwamba, ni Muumba tu—Mungu Yule wa Kipekee—ambaye anaonyeshwa kwa njia hii na ndiye aliye na hali halisi hii. Kwa nini tuzungumzie mamlaka ya Mungu? Mamlaka ya Mungu Mwenyewe yanatofautiana vipi na mamlaka yaliyomo kwenye akili ya binadamu? Ni nini maalum sana kuyahusu? Na kuna umuhimu gani haswa kuyazungumzia hapa? Kila mmoja wenu lazima aweze kutilia maanani kwa umakinifu suala hili. Kwa watu wengi zaidi, “Mamlaka ya Mungu” ni fikira isioeleweka, ile ambayo ni ngumu sana kupata kuielewa, na mazungumzo yoyote kuihusu huenda yasizae matunda mazuri. Kwa hivyo lazima kutakuwepo na pengo kati ya maarifa ya mamlaka ya Mungu ambayo binadamu anaweza kumiliki, na hali halisi ya mamlaka ya Mungu. Ili kuliziba

pengo hili, mtu lazima kwa utaratibu aweze kuelewa mamlaka ya Mungu kwa njia ya watu halisi maishani, matukio, vitu au mambo muhimu yanayopatikana katika uwezo wa binadamu, na ambayo binadamu wanaweza kuyaelewa. Ingawaje kauli hii “Mamlaka ya Mungu” inaweza kuonekana kama isiyoeleweka, mamlaka ya Mungu kwa kweli si ya dhahania kamwe. Yeye yupo na binadamu kila dakika ya maisha yake, akimwongoza kila siku. Kwa hivyo, katika maisha ya kila siku ya kila mtu ataweza haswa kuona na kupitia dhana halisi ya mamlaka ya Mungu. Uhalisi huu ni ithibati tosha kwamba mamlaka ya Mungu kwa kweli yapo, na unakuruhusu kabisa kutambua na kuelewa hoja hii kwamba Mungu anamiliki mamlaka haya.

Mungu aliumba kila kitu, na baada ya kukiumba, Anao utawala juu ya kila kitu. Kuongezea kuwa na utawala juu ya kila kitu, pia anadhibiti kila kitu. Wazo hili linamaanisha nini “Mungu anadhibiti kila kitu”? Hali hii inaweza kuelezewa vipi? Hali hii inatumika vipi katika maisha halisi? Mnawezaje kuyajua mamlaka ya Mungu kwa kuelewa hoja hii kwamba “Mungu Anadhibiti kila kitu”? Kutoka kwenye kauli ile ile “Mungu anadhibiti kila kitu” tunafaa kuona kwamba kile ambacho Mungu anadhibiti si sehemu ya sayari, sehemu ya uumbaji, wala sehemu ya mwanadamu, lakini kila kitu: kuanzia kwa viumbe vile vikubwa hadi vile vidogovidogo, kuanzia kwa vile vinavyoonekana hadi visivyooonekana, kuanzia kwa nyota ulimwenguni hadi kwenye vitu vilivyo na uhai ulimwenguni, pamoja na viumbe vidogovidogo visivyoweza kuonekana kwa macho ya kawaida au viumbe vilivyo katika maumbo mengine. Huu ndio ufafanuzi hakika wa “kila kitu” ambacho Mungu “anadhibiti,” na ndio upana ambao Mungu anaonyesha ukuu Wake, urefu wa utawala na kanuni Yake.

Kabla ya binadamu hawa kujitokeza, viumbe vyote—sayari zote, nyota zote kule mbinguni—tayari vilikuwepo. Kwenye kiwango cha vitu vikubwa, vyombo hivi vya mbinguni vimekuwa vikizunguka mara kwa mara chini ya udhibiti wa Mungu, kwa uwepo wavyo wote, hata hivyo miaka mingi imepita. Ni sayari gani inaenda wapi na wakati gani haswa; ni sayari gani inafanya kazi gani, na lini; ni sayari gani inazunguka katika mzingo gani, na ni lini inatoweka au inabadilishwa—vitu hivi vyote vinasonga mbele bila ya kosa lolote dogo. Nafasi za sayari na umbali kati yazo ni masuala yanayofuata ruwaza maalum, ni masuala ambayo yanaweza kufafanuliwa kwa data yenye uhakika; njia ambazo zinasafiria, kasi na ruwaza ya mizingo yao, nyakati ambapo zinapatikana kwenye nafasi mbalimbali zinaweza kufafanuliwa kwa hakika na kufafanuliwa kwa sheria maalum. Kwa miaka na mikaka sayari zimefuata sheria hizi na hazijawahi kupotoka hata chembe. Hakuna nguvu inaweza kubadilisha au kutatiza mizingo yazo au ruwaza zao ambazo zinafuata. Kwa sababu sheria maalum zinazotawala mzunguko wazo na data yenye uhakika inayozifafanua iliamuliwa kabla na mamlaka ya Muumba, zinatii sheria hizi zenyewe, kulingana na ukuu na udhibiti wa Muumba. Kwenye kiwango cha mambo makubwamakubwa, si vigumu kwa binadamu kujua zaidi kuhusu ruwaza

fulani, data fulani, pamoja na sheria au matukio fulani yasiyoeleweka au yasiyoelezeka. Ingawaje binadamu hawakubali kwamba Mungu yupo, haukubali hoja kwamba Muumba aliumba na anatawala kila kitu na zaidi ya yote hautambui uwepo wa mamlaka ya Muumba, wanasayansi wa kibinadamu, wanafalaki, nao wanafizikia wanachunguza na kugundua zaidi na zaidi kwamba uwepo wa kila kitu kwenye ulimwengu, na kanuni na ruwaza zinazoonyesha mzunguko wavyo, vinatawaliwa na kudhibitiwa na nishati nyeusi kubwa na isiyoonekana. Hoja hii inampa binadamu mshawasha wa kukubaliana na kutambua kwamba kunaye Mwenyezi aliye miongoni mwa ruwaza hizi za mzunguko, anayepangilia kila kitu. Nguvu zake si za kawaida, na ingawaje hakuna anayeweza kuona uso Wake wa kweli, Yeye hutawala na kudhibiti kila kitu kila dakika. Hakuna binadamu au nguvu zozote zile zinazoweza kuuzidi ukuu Wake. Huku binadamu akiwa amekabiliwa na hoja hii, lazima atambue kwamba sheria zinazotawala uwepo wa kila kitu haziwezi kudhibitiwa na binadamu, haziwezi kubadilishwa na yeyote; na wakati uo huo binadamu lazima akubali kwamba, binadamu hawezi kuelewa kikamilifu sheria hizi. Na hizi sheria hazitokei kiasili lakini zinaamrisha na Bwana na Mungu. Haya yote ni maonyesho na mamlaka ya Mungu yanayoonyesha kwamba mwanadamu anaweza kuelewa katika kiwango cha mambo makubwa.

Kwenye kiwango cha mambo madogomadogo, milima, mito, maziwa, bahari, na maeneo ya ardhi yote ambayo binadamu anatazama nchini, misimu yote ambayo yeye anapitia, mambo yote yanayopatikana kwenye ulimwengu, kukiwemo mimea, wanyama, vijiumbe na binadamu, vyote viko chini ya ukuu wa Mungu na vinadhitiwa na Mungu Mwenyewe. Katika ukuu na udhibiti wa Mungu, vitu vyote vinakuwepo au vinatoweka kulingana na fikira Zake, maisha ya vitu hivi yanatawaliwa na sheria fulani, na vinakua na kuzaana kulingana nazo. Hakuna binadamu au kiumbe chochote kilicho juu ya sheria hizi. Kwa nini hali iko hivi? Jibu la pekee tu ni, kwa sababu ya mamlaka ya Mungu. Au, nikijibu kwa njia nyingine, kwa sababu ya fikira za Mungu na matamshi ya Mungu; kwa sababu Mungu Mwenyewe hufanya haya yote. Hivi ni kusema, ni mamlaka ya Mungu na ni akili ya Mungu ambayo iliunda sheria hizi; zitasonga na kubadilika kulingana na fikira Zake, na kusonga huku na mabadiliko haya yote yanafanyika au kutoweka kwa minajili ya mpango Wake. Hebu tuchukulie magonjwa ya mlipuko, kwa mfano. Yanazuka tu bila onyo, hakuna anayejua asili yake, au sababu maalum zinazoelezea ni kwa nini huwa yanafanyika, na kila wakati magonjwa ya mlipuko yanapofika mahali fulani, wale walio na bahati mbaya hawawezi kukwepa maafa. Sayansi ya binadamu inafafanua na kutuelewesha kwamba magonjwa ya mlipuko yanasababishwa na kuenea kwa vijiumbe maradhi vibaya au haribifu, na kasi yao, eneo lao, na mbinu ya kuenea kwake haiwezi kutabiriwa au kudhibitiwa na sayansi ya binadamu. Ingawaje binadamu huvipinga vijiumbe maradhi hivi kwa kila namna inayowezezekana, huwa hauwezi kudhibiti ni watu gani au wanyama gani ambao wanaathiriwa

kwa vyovyote vile wakati kunapokuwa na mkurupuko wa magonjwa mlipuko. Kitu cha pekee ambacho binadamu wanaweza kufanya ni kujaribu kuyazuia, kuyapinga, na kuyafanyia utafiti. Lakini hakuna anayejua chanzo asilia kinachoelezea mwanzo au mwisho wa magonjwa mlipuko yoyote ya kibinafsi, na hakuna anayeweza kuyadhibiti. Wakiwa wamekabiliwa na ongezeko na kuenea kwa magonjwa mlipuko, suala la kwanza ambalo binadamu hufanya ni kuunda chanjo, lakini mara nyingi magonjwa mlipuko hayo hutoweka kabisa kabla ya hata chanjo kuwa tayari. Kwa nini magonjwa mlipuko hutoweka kabisa? Wengine husema kwamba viini vimeweza kudhibitiwa, wengine husema kwamba vimetoweka kabisa kwa sababu ya mabadiliko katika misimu.... Kuhusiana na ikiwa makisio haya ya kuchanganyikiwa ni kweli au la, sayansi haiwezi kutupa ufafanuzi wowote, na wala haitoi jibu lolote lenye uhakika. Kile ambacho binadamu wanakabiliwa nacho si makisio haya tu lakini pia ukosefu wa mwanadamu katika kuelewa na woga wa magonjwa mlipuko haya. Hakuna anayejua, baada ya kila kitu kuchambuliwa, ni kwa nini magonjwa mlipuko haya huanza au ni kwa nini huisha. Kwa sababu binadamu wanayo imani tu katika sayansi, unategemea pakubwa kwa sayansi hiyo, lakini hautambui mamlaka ya Muumba au kuukubali ukuu Wake, hautawahi kuwa na jibu.

Katika ukuu wa Mungu, vitu vyote vinazaana, vinakuwepo, na huangamia kwa sababu ya mamlaka Yake na usimamizi Wake. Baadhi ya mambo huja na kwenda polepole, na binadamu hawezi kutambua ni wapi yalitokea au kung'amua sheria ambazo mambo haya hufuata, sisemi hata kuelewa sababu za mambo haya kuja na kwenda. Ingawaje binadamu anaweza kushuhudia, kusikia, au kupitia yote yanayokuja na kuisha miongoni mwa mambo yote; ingawaje mambo haya yanao mwelekeo kwa binadamu, na ingawaje binadamu hung'amua kupitia kwa yaliyofichika akilini mwake, hali isiyokuwa ya kawaida, hali ya mara kwa mara au hata hali ya ajabu ya mambo mbalimbali, bado hajui chochote kuhusu mapenzi ya Muumba na akili Yake ambavyo vinaelezea mambo hayo. Kunazo hadithi nyingi zinazotokana na haya mambo yote, ukweli mwingi uliofichwa. Kwa sababu binadamu amepotoka na kwenda mbali na Muumba, kwa sababu hakubali hoja hii kwamba Mamlaka ya Muumba ndiyo hutawala mambo yote, hatawahi kujua kila kitu kinachofanyika katika ukuu Wake. Kwa sehemu nyingi zaidi, udhibiti na ukuu wa Mungu huzidi mipaka ya fikra ya binadamu, maarifa ya binadamu, kuelewa kwa binadamu, kuhusu kile ambacho sayansi ya binadamu inaweza kutimiza; uwezo wa binadamu walioundwa hauwezi kushindana nao. Baadhi ya watu husema "Kwa sababu hujashuhudia ukuu wa Mungu wewe mwenyewe, unawezaje kusadiki kwamba kila kitu kinatokana na mamlaka Yake?" Kuona si kuamini kila mara; kuona si kutambua na kuelewa kila mara. Kwa hivyo sadiki hutokea wapi? Ninaweza kusema kwa uhakika, "Sadiki inatokana na kiwango na kina cha kuelewa kwa watu kwa, na hali wanayopitia wao, uhalisi na chanzo kikuu cha mambo." Kama unasadiki kwamba Mungu yupo, lakini huwezi kutambua, na wala huwezi kuelewa, hoja ya

udhibiti wa Mungu na ukuu wa Mungu katika mambo yote, basi katika moyo wako hutawahi kukubali kwamba Mungu anayo mamlaka kama haya na kwamba mamlaka ya Mungu ni ya kipekee. Hutawahi kukubali kwa kweli Muumba kuwa Bwana wako, Mungu wako.

Hatima ya Binadamu na Hatima ya Ulimwengu Haviwezi Kutenganishwa na Ukuu wa Muumba

Nyinyi nyote ni watu wazima. Baadhi yenu ni wa umri wa kati; baadhi mmefikisha umri wa uzee. Kutoka kwa yule asiyesadiki hadi kwa yule anayesadiki, na kuanzia mwanzo wa kusadiki kwa Mungu hadi kukubali neno la Mungu na kuweza kupitia kazi ya Mungu, je, ni maarifa kiwango kipi mliyopata kuuhusu ukuu wa Mungu? Ni maono yapi mliyopata kwenye hatima yenu ya kuwa binadamu? Je, mtu anaweza kutimiza kila kitu anachotamani katika maisha? Je, ni mambo mangapi kwenye miongo michache iliyopita katika kuwepo kwenu mliyoweza kutimiza kama mlivyopenda? Ni mambo mangapi hayafanyiki kama yalivyotarajiwa? Ni mambo mangapi hutupata kwa mshangao mzuri? Ni mambo mangapi ambayo ungali unasubiri kutimia—unasubiri bila kufahamu muda sahihi, unasubiria mapenzi ya Mbinguni? Mambo mangapi yanakufanya uhisi kana kwamba huna wa kukusaidia na umezuiliwa? Watu wote wanayo matumaini kuhusu hatima yao, na hutarajia kwamba kila kitu katika maisha yao kitaenda sawa na wanavyopenda, kwamba hawatakosa chakula wala mavazi, kwamba utajiri wao utaongezeka pakubwa. Hakuna anayetaka maisha ya kimaskini na ya taabu, yaliyojaa ugumu, na kuandamwa na majanga. Lakini watu hawawezi kuona mbele au kudhibiti mambo haya. Pengine kwa baadhi ya watu, yaliyopita ni mchanganyiko tu wa yale mambo waliyoyapitia; hawajifunzi katu ni nini mapenzi ya Mbinguni, wala hawajali mapenzi hayo ni yapi. Wanaishi kwa kudhihirisha maisha yao bila kufikiria, kama wanyama, wakiishi siku baada ya siku, bila kujali kuhusu hatima ya binadamu ni nini, kuhusu ni kwa nini binadamu wako hai au vile wanavyostahili kuishi. Watu hawa hufikia umri wa uzee bila ya kufaidi ufahamu wowote wa hatima ya binadamu, na mpaka wakati ule wanapokufa hawana habari yoyote kuhusu maana ya maisha. Watu kama hao wamekufa; ni viumbe bila roho; wao ni wanyama. Ingawaje katika kuishi miongoni mwa mambo haya yote, watu hupata furaha kutoka kwa njia nyingi ambazo ulimwengu hutosheleza mahitaji yao ya anasa, ingawaje wanauona ulimwengu huu wa anasa ukiwa unapiga hatua bila kusita, hali yao binafsi waliyoipitia—kile ambacho mioyo yao na roho zao zinahisi na kupitia—hakina uhusiano wowote na mambo ya anasa, na hakuna kitu chochote cha anasa ambacho kinaweza kuchukua nafasi yake. Ni utambuzi ndani ya moyo wa mtu, kitu ambacho hakiwezi kuonekana kwa jicho vivyo hivyo tu. Utambuzi huu umo katika ufahamu wa mtu wa, na hisia za mtu za, maisha ya binadamu na hatima ya binadamu. Na mara nyingi humwongoza mtu katika kuelewa kwamba Bwana yule asiyeonekana anapanga vitu vyote, Anaunda kila kitu kwa ajili ya binadamu. Katikati ya haya yote, mtu hawezi kuepuka ila kukubali mipangilio na mipango ya

hatima ya mambo; wakati uo huo, mtu hawezi kuepuka ila kukubali njia iliyo mbele ambayo Muumba amempangia, ukuu wa Muumba dhidi ya hatima ya mtu. Hii ndiyo hoja isiyopingika. Haijalishi ni maono na mtazamo gani ambao mtu anao kuhusu hatima yake, hakuna anayeweza kubadilisha hoja hii.

Pale utakapoenda kila siku, kile utakachofanya, yule au kile utakachokumbana nacho, kile utakachosema, kile kitakachokufanyikia—je, kati ya vyote hivi kipo kinachoweza kutabirika? Watu hawawezi kutabiri matukio haya yote, sikutajii kudhibiti namna ambavyo yanavyoendelea. Katika maisha, matukio haya yasiyotabirika hufanyika kila wakati, na ni tukio la kila siku. Mabadiliko haya ya kila siku na njia ambazo yanajitokeza, au ruwaza ambazo yanajitokeza, ni vikumbusho vya kila wakati kwa binadamu kwamba hakuna kinachofanyika bila mpango, kwamba njia ya maendeleo inayochukuliwa na mambo haya, na kutoepukika kwa mambo haya, haviwezi kubadilishwa na mapenzi ya binadamu. Kila tukio linaonyesha onyo kutoka kwa Muumba kwa mwanadamu, na pia linatuma ujumbe kwamba, binadamu hawawezi kudhibiti hatima zao wenyewe; na wakati uo huo kila tukio ni upingaji wa malengo yasiyo na mwelekeo, yasiyo na maana ya binadamu na tamanio la kuchukua hatima yake na kutaka kuidhibiti mwenyewe. Ni sawa na makofi yenye nguvu juu ya masikio ya binadamu moja baada ya jingine, yanayolazimisha binadamu kufikiria upya ni nani, hatimaye, atatawala na kudhibiti hatima yao. Na kama vile malengo na matamano yao yanavyokiukwa mara kwa mara na kusambaratika, binadamu kwa kawaida huishia kukubali kwa nadharia yao bila kufahamu kile ambacho hatima yao imesheheni, kukubali kwa uhalisi, kwa mapenzi ya Mbinguni na ukuu wa Muumba. Kutokana na mabadiliko haya ya kila siku katika hatima za maisha yote ya binadamu, hakuna kitu ambacho hakifichui mipango ya Muumba na ukuu Wake; hakuna kile ambacho hakiutumi ujumbe huu kwamba “yale mamlaka ya Muumba hayawezi kupitwa,” ambacho hakionyeshi ukweli wa milele kwamba “mamlaka ya Muumba ni ya juu zaidi.”

Hatima za binadamu na zile za ulimwengu zimeingiliana kwa ndani na ukuu wa Muumba, zimefungamanishwa na haziwezi kutenganishwa na mipango ya Muumba; na hatimaye, haziwezi kutenganishwa na mamlaka ya Muumba. Kupitia kwenye sheria za mambo yote binadamu huja kuelewa mipango ya Muumba na ukuu Wake; kupitia kwenye sheria za namna ya kuishi ambazo anaona katika utawala wa Muumba; kutoka kwenye hatima za mambo yote anapata hitimisho kuhusu njia ambazo Muumba huonyesha ukuu Wake na kuvidhibiti; na kwenye mzunguko wa maisha ya binadamu na mambo yote ambayo binadamu kwa kweli hupitia ile mipango na mipangilio ya Muumba kwa mambo yote na kwa viumbe vyote vilivyo hai na anashuhudia kwa kweli namna ambavyo mipango na mipangilio hiyo inavyozidi sheria zote za nchi, kanuni, na taasisi, mamlaka na nguvu zote nyingine. Kwa mujibu wa haya, binadamu wanashawishiwa kutambua kwamba, ukuu wa Muumba hauwezi kukiukwa na kiumbe chochote kilichoumbwa,

kwamba hakuna nguvu zinazoweza kuharibu au kubadilisha matukio na mambo yaliyoamuliwa kabla na Muumba. Ni kupitia kwenye sheria na kanuni hizi takatifu ambapo binadamu na viumbe vyote wanaweza kuishi na kuzalisha, kizazi baada ya kizazi. Je, huu si mfano halisi wa mamlaka ya Muumba? Ingawaje binadamu huona, kwenye sheria zile za malengo, ukuu wa Muumba na utaratibu Wake wa matukio yote na mambo yote, ni watu wangapi wanaweza kung'amua kanuni ya ukuu wa Muumba juu ya ulimwengu? Ni watu wangapi wanaweza kujua, kutambua, kukubali kwa kweli na kujinyenyekeza kwa ukuu na mpangilio wa Muumba dhidi ya hatima zao wenyewe? Nani, ambaye baada ya kusadiki hoja ya ukuu wa Muumba juu ya viumbe vyote, ataweza kusadiki kwa kweli na kutambua kwamba Muumba pia anaamrisha hatima hii ya maisha ya binadamu? Ni nani anayeweza kuelewa kwa kweli hoja hii kwamba hatima ya binadamu imo kwenye kiganja cha mkono wa Muumba? Aina ya mtazamo ambao binadamu wanafaa kuchukua katika ukuu wa Muumba, wanapokabiliwa na hoja kwamba Anatawala na kudhibiti hatima ya binadamu, ni uamuzi ambao kila binadamu ambaye kwa sasa anakabiliwa na hoja hii lazima ajiamulie mwenyewe.

Awamu Sita katika Maisha ya Binadamu

Katika mkondo wa maisha ya mtu, kila mtu hufikia kwenye misururu ya awamu muhimu. Hizi ni hatua za kimsingi zaidi, na muhimu zaidi, zinazoamua hatima ya maisha ya mtu. Kile kinachofuata ni ufafanuzi mfupi kuhusu mafanikio haya ambayo kila mtu lazima apitie kwenye mkondo wa maisha yake.

Kuzaliwa: Awamu ya Kwanza

Mahali ambapo mtu amezaliwa, ni familia gani alimozaliwa, jinsia ya mtu, umbo la mtu, na wakati wa kuzaliwa—haya ndiyo maelezo ya awamu ya kwanza ya maisha ya binadamu.

Hakuna yeyote aliye na chaguo kuhusu sehemu hizi za awamu hii; zote ziliamuliwa kabla, mapema kabisa na Muumba. Haziathiriwi na mazingira ya nje kwa vyovyote vile, na hakuna masuala yanayosababishwa na binadamu yanaweza kubadilisha hoja hizi ambazo Muumba aliamua kabla. Kwa mtu kuweza kuzaliwa inamaanisha kwamba Muumba tayari ametimiza hatua ya kwanza ya hatima ambayo Amempangilia mtu huyo. Kwa sababu Aliamua kabla maelezo haya yote tena mapema mno, hakuna aliye na nguvu za kubadilisha maelezo yoyote yale. Licha ya hatima ya baadaye ya mtu, hali za kuzaliwa kwa mtu ziliamuliwa kabla, na zinabakia kama zilivyo; haziathiriwi kwa njia yoyote ile na hatima ya mtu katika maisha, wala haziathiri kwa vyovyote vile ukuu wa Muumba juu yazo.

1. Maisha Mapya Yanazaliwa Kulingana na Mipango ya Muumba

Ni maelezo yapi ya awamu ya kwanza—mahali mtu anapozaliwa, familia ya mtu, jinsia ya mtu, umbo la mwili wa mtu, muda wa kuzaliwa kwa mtu—ambayo mtu anaweza kuchagua? Bila shaka, kuzaliwa kwa mtu ni tukio asiloweza kuchagua: Mtu anazaliwa bila hiari yake, katika mahali fulani, muda fulani, kwenye familia fulani, akiwa na umbo fulani la kimwili; mtu anakuwa mmojawapo wa familia fulani bila hiari, anarithi kizazi fulani cha familia. Mtu hana chaguo kwenye awamu hii ya kwanza ya maisha, lakini anazaliwa kwenye mazingira yanayochaguliwa kulingana na mipango ya Muumba, kwenye familia mahususi, na jinsia na umbo mahususi, kwenye wakati mahususi ambao unaunganishwa kwa undani na mkondo wa maisha ya mtu huyu. Mtu anaweza kufanya nini katika awamu hii muhimu? Yote yakisemwa, kwa kweli mtu hana chaguo kuhusu maelezo yoyote yale yanayohusu kuzaliwa kwake. Kama isingekuwa kuamua kabla kwa Muumba na mwongozo Wake, mtu aliyezaliwa upya kwenye ulimwengu huu asingejua ni wapi atakapoenda au ni wapi atakapoishi, asingekuwa na mahusiano yoyote, asingekuwa na popote na asingekuwa na maskani yoyote halisi. Lakini kwa sababu ya mipangilio makinifu ya Muumba, anaanza safari ya maisha yake akiwa na mahali pa kuishi, wazazi, na mahali anapoita nyumbani na watu wa ukoo. Kotekote kwenye mchakato huu, mwanzo wa maisha haya mapya unaamuliwa na mipango ya Muumba, na kila kitu ambacho mtu huyu atakuja kumiliki ataweza kukabidhiwa na Muumba. Kutoka kwenye kiumbe kinachoelea kisichokuwa na jina lolote hadi kinapoanza kuwa na nyama na damu polepole, kinachoweza kuonekana, na hatimaye kuwa binadamu anayeweza kushikika, mojawapo ya viumbe vya Mungu, anayefikiria, anayepumua, anayehisi joto na baridi, anayeshiriki katika shughuli za kawaida za kiumbe kilichoumbwa kwenye ulimwengu yakinifu na ambaye atapitia mambo haya yote ambayo kiumbe kilichoumbwa lazima kipitie maishani. Kule Kuamuliwa kabla kwa kuzaliwa kwa mtu na Muumba kunamaanisha kwamba ataweza kumpa mtu huyu mambo yote yanayohitajika kwa kuishi kwake; na kwamba mtu anazaliwa vilevile inamaanisha kwamba yeye atapokea mambo yote yanayohitajika kutoka kwa Muumba, kwamba kuanzia wakati ule kwenda mbele yeye ataishi katika umbo jingine, linalotolewa na Muumba na linalotii ukuu wa Muumba.

2. Kwa Nini Binadamu Tofauti Wanazaliwa Katika Hali Tofauti

Mara nyingi watu wanapenda kufikiria kwamba, kama wangezaliwa tena, wangezaliwa kwenye familia maarufu; kama wangukuwa wanawake, wangufanana na Binti wa Kifalme Anayependeza na wangupendwa na kila mtu, na wangezaliwa wanaume, wangukuwa Kaka Mwenye Mvuto na Haiba, wasikose mahitaji yoyote, huku ulimwengu mzima ukiwaitikia mara moja kila unapoitwa na wao. Mara nyingi kuna wale walio na picha nyingi kuhusu kuzaliwa kwao na huwa hawajatosheka kabisa na huko kuzaliwa kwao, wanachukia familia zao, umbo lao, jinsia yao, na hata wakati wa kuzaliwa kwao. Ilhali watu hawajawahi kuelewa ni kwa nini wamezaliwa katika familia fulani au kwa nini wanafanana jinsi fulani. Hawajui kwamba, licha

ya ni wapi wamezaliwa au ni vipi wanavyoonekana, wanafaa kuendeleza wajibu mbalimbali na kutimiza kazi maalum tofautitofauti katika usimamizi wa Muumba—kusudi hili halitawahi kubadilika. Ingawa katika macho ya Muumba, mahali anapozaliwa mtu, jinsia ya mtu, umbo la mwili wa mtu hivi vyote ni vitu vya muda. Ni misururu ya mambo madogomadogo katika kila awamu ya usimamizi Wake wa mwanadamu kwa ujumla. Na hatima halisi ya mtu na mwisho wake vyote haviamuliwi kutokana na wapi ambapo yeye amezaliwa katika awamu yoyote ile, lakini vinaamuliwa na kazi maalum ambayo yeye atatekeleza katika kila maisha, kwa hukumu ya Muumba kwao wakati ambapo usimamizi Wake wa mpango vitakamilika.

Inasemekana kwamba kunayo sababu katika kila athari, na kwamba hakuna athari ambayo haina sababu. Na kwa hivyo kuzaliwa kwa mtu kumefungamanishwa haswa na maisha yake ya sasa na yale ya awali. Kama kifo cha mtu kinasitisha awamu yake ya sasa ya maisha, basi kuzaliwa kwa mtu ndio mwanzo wa mzunguko mpya; kama mzunguko wa kale unawakilisha maisha ya awali ya mtu, basi mzunguko huo mpya kwa kawaida ndio maisha yao ya sasa. Kwa sababu kuzaliwa kwa mtu kunaunganishwa na maisha ya kale ya mtu huyu pamoja na maisha ya sasa ya mtu huyu, mahali anapoishi, familia yake, jinsia, umbo na mambo mengine kama hayo, ambayo yanahusiana na kuzaliwa kwa mtu, vyote vinahusiana na mambo yote. Hii inamaanisha kwamba, mambo yanayoathiri kuzaliwa kwa mtu hayaathiriwi tu na maisha ya awali ya mtu, lakini yanaamuliwa na hatima ya mtu katika maisha ya sasa. Hii inaelezea mseto wa hali tofauti ambazo watu wanazaliwa: Baadhi wanazaliwa katika familia fukara, wengine katika familia tajiri. Baadhi wanazaliwa katika kundi la watu wa kawaida, wengine wanazaliwa katika ukoo wa kipekee. Baadhi wanazaliwa kusini, wengine wanazaliwa kaskazini. Baadhi wanazaliwa jangwani na wengine wanazaliwa katika ardhi zenye rotuba. Kuzaliwa kwa baadhi ya watu kunaandamana na vifijo, vicheko, na sherehe, wengine wanaleta machozi, janga, na matatizo. Baadhi wanazaliwa ili wathaminiwe, wengine wawekwe pembeni kama magugu. Baadhi wanazaliwa wakiwa na heshima na staha na wengine wanazaliwa wakiwa na mikosi na mikasa. Baadhi wanapendeza kuwatazama, na wengine wanatisha kuwatazama. Baadhi wanazaliwa usiku wa manane, wengine wanazaliwa chini ya jua kali la utosi. ... Kuzaliwa kwa watu wa kila aina kunaamuliwa na hatima ambazo Muumba ameweka kwa ajili yao; kuzaliwa kwao kunaamua hatima zao katika maisha ya sasa pamoja na wajibu ambao wataendeleza na kazi maalum watakazotimiza. Yote haya yanategemea ukuu wa Muumba, ulioamuliwa kabla na Yeye; hakuna anayeweza kukimbia kundi hili lao lililoamuliwa kabla, hakuna anayeweza kubadilisha kuzaliwa kwao, na hakuna anayeweza kuchagua hatima yake binafsi.

Kukua: Awamu ya Pili

Kutegemea na aina gani ya familia ambayo wamezaliwa ndani, watu hukua katika

mazingira tofauti ya nyumbani na wakajifunza mafunzo tofauti kutoka kwa wazazi wao. Hali hizi huamua masharti ambayo mtu anafikisha umri wa kubaleghe na kukua inawakilisha awamu ya pili muhimu ya maisha ya mtu. Inajulikana kwamba, watu hawana chaguo katika awamu hii, vilevile. Hii pia imepangwa, ilipangwa kabla.

1. Hali Ambazo Mtu Hukulia Ndani Zimepangwa na Muumba

Mtu hawezi kuchagua watu, matukio au vitu anavyoadilishwa na kushawishiwa navyo anapokua. Mtu hawezi kuchagua ni maarifa au mbinu gani atapata, ni mazoea gani ataishia kuwa nayo. Mtu hana kauli kuhusiana na wazazi na watu wake wa ukoo, aina ya mazingira ambayo atakulia ndani; mahusiano yake na watu, matukio, na mambo yaliyo katika mazingira yake na namna yanavyoathiri maendeleo yake, vyote ni zaidi ya udhibiti wake. Ni nani anayeamua mambo haya, basi? Ni nani anayeyapangilia? Kwa sababu watu hawana chaguo katika suala hili, kwa vile hawawezi kuamua mambo haya wao wenyewe, na kwa sababu bila shaka hayajipangi yenyewe kwa kawaida, ni wazi kabisa kwamba kuundwa kwa watu, matukio na vitu hivi vyote kunategemea mikono ya Muumba. Bila shaka, kama vile tu Muumba anavyopanga hali fulani za kuzaliwa kwa kila mtu, Yeye hupangilia pia hali mahususi ambazo mtu hukulia. Kama kuzaliwa kwa mtu kutaleta mabadiliko kwa watu, kwa matukio, na mambo yanayomzunguka yeye, basi kukua na maendeleo ya mtu huyo vyote vitaweza kuwaathiri vilevile. Kwa mfano, baadhi ya watu wanazaliwa katika familia fukara, lakini wanalelewa wakiwa wamezungukwa na utajiri; wengine wanazaliwa katika familia tajiri lakini husababisha utajiri wa familia zao kupungua, kiasi cha kwamba wanalelewa katika mazingira ya kimaskini. Hakuna kuzaliwa kwa yeyote kunatawaliwa na kanuni isiyobadilika, na hakuna anayelelewa katika hali zisizozuilika, na zisizobadilika. Haya si mambo ambayo binadamu anaweza kufikiria au kudhibiti; mambo haya yote ni mazao ya hatima ya mtu, na yanaamuliwa na hatima ya mtu. Bila shaka, kimsingi ni kwamba yote haya yaliamuliwa kabla katika hatima ya mtu na Muumba, yanaamuliwa na ukuu wa Muumba juu ya, na mipango Yake ya, hatima ya mtu huyu.

2. Hali Mbalimbali Ambazo Watu Hukulia Ndani Husababisha Wajibu Tofauti

Hali za kuzaliwa kwa mtu huanzisha katika kiwango cha kimsingi mazingira na hali ambazo hukulia ndani, na hali ambazo mtu hukulia ndani vilevile ni zao la hali za kuzaliwa kwake. Kwenye wakati huu mtu anaanza kujifunza lugha, na akili za mtu zinaanza kukumbana na kuchanganua mambo mengi mapya, na katika mchakato huu mtu anakua bila kusita. Mambo ambayo mtu anasikia kwa masikio yake, anaona kwa macho yake, na anang'amua kwa akili zake huboresha na kuhuisha kwa utaratibu ulimwengu wa ndani wa mtu. Watu, matukio, na mambo ambayo mtu anakumbana nayo, maarifa ya kawaida, maarifa, na mbinu anazojifunza, na njia za kufikiria ambazo mtu anaathiriwa nazo, anaambiwa au kufunzwa, vyote vitamwongoza na

kuathiri hatima ya maisha yake. Lugha anayojifunza mtu anapokua na njia yake ya kufikiria haviwezi kutenganishwa kutoka kwenye mazingira ambayo yeye analelewa katika ujana wake, na hayo mazingira yana wazazi, ndugu zake, na watu wengine, matukio, na mambo yanayomzunguka. Kwa hivyo mkondo wa maendeleo ya mtu unaamuliwa na mazingira ambayo yeye anakulia ndani, na pia unategemea watu, matukio, na mambo ambayo mtu anakumbana nayo kwenye kipindi hiki cha muda. Kwa sababu masharti ambayo mtu hukulia ndani yaliamuliwa kabla na tena mapema mno, mazingira anayoishi kwenye mchakato huu pia, kwa kawaida, yaliamuliwa kabla. Hayaamuliwi na chaguo na mapendeleo ya mtu, lakini yanaamuliwa kulingana na mipango ya Muumba, yanaamuliwa na mipangilio makinifu ya Muumba, na ukuu wa Muumba juu ya hatima ya mtu huyo katika maisha. Kwa hivyo watu ambao mtu yeyote hukumbana nao katika mkondo wa kukua, na mambo ambayo mtu hukutana nayo, vyote vimeunganishwa bila kuzuilika kwa mipango na mipangilio ya Muumba. Watu hawawezi kutabiri aina hizi za mahusiano mapevu, wala hawawezi kuyadhibiti au kuweza kuyaelewa. Mambo mengi tofauti na watu wengi tofauti wanao mwelekeo wa mazingira ambayo mtu hukulia, na hakuna binadamu anaweza kupangilia na kupanga mtandao mpana kama huo wa muunganisho. Hakuna mtu au kitu isipokuwa Muumba anaweza kudhibiti kujitokeza, kuwepo, na kutoweka kwa watu mbalimbali, matukio na mambo, na ni mtandao mpana ajabu wa muunganisho unaounda maendeleo ya mtu kama ilivyoamuliwa kabla na Muumba, na kuunda mazingira tofauti ambayo watu wanakulia ndani, na kuunda wajibu mbalimbali unaohitajika kwa minajili ya kazi ya Muumba ya usimamizi, kuweka misingi thabiti, yenye nguvu ili watu waweze kukamilisha kwa ufanisi kazi yao maalum.

Uhuru: Awamu ya Tatu

Baada ya mtu kupita utoto na wakati wake wa kubaleghe na kwa utaratibu bila kuzuilika kufikia ukomavu, hatua inayofuata ni kwake yeye kuachana kabisa na ujana wake, kuwaaga wazazi wake, na kukabiliana na barabara iliyo mbele yake akiwa mtu mzima huru. Wakati huo, lazima wakabiliane na watu, matukio na mambo yote ambayo mtu mzima lazima apitie, na kukabiliana na sehemu zote za hatima yake ambazo zitajiwasilisha hivi karibuni. Hii ndiyo awamu ya tatu ambayo lazima mtu apitie.

1. Baada ya Kuwa Huru, Mtu Huanza Kupitia Ukuu wa Muumba

Kama kuzaliwa kwa mtu na kulelewa kwake ni “kipindi cha matayarisho” katika safari ya mtu maishani, kuweka lile jiwe la msingi katika hatima ya mtu, basi uhuru wa mtu ndio mazungumzo nafsi ya kufungua hatima ya maisha ya mtu. Kama kuzaliwa na kukua kwa mtu ni utajiri ambao wameweza kulimbikiza kwa minajili ya hatima yao maishani, basi uhuru wa mtu huyo unaanza wakati ule wanaanza kutumia au kuongeza utajiri huo. Wakati mtu anawaacha

wazazi na kuwa huru, masharti ya kijamii ambayo anakabiliana nayo, na aina ya kazi na ajira inayopatikana kwa mtu, vyote vinaamriwa na hatima na havina uhusiano wowote na wazazi wa mtu. Baadhi ya watu huchagua kozi nzuri katika chuo na huishia kupata kazi ya kutosheleza baada ya kuhitimu, na hivyo basi kupiga hatua ya kwanza ya mafanikio katika safari yao ya maisha. Baadhi ya watu hujifunza na kumiliki mbinu nyingi tofauti na ilhali hawapati kazi katu ambayo inawafaa au hawapati cheo chao, bila kutaja kwamba hawana ajira yoyote; wakati wa safari ya maisha yao wanajipata wakiwa wamekwazwa katika kila kona, wameandamwa na matatizo, matumaini yao madogo na maisha yao hayana uhakika. Baadhi ya watu wanatia bidii katika masomo yao, ilhali wanakosa kwa karibu sana fursa zao zote za kupokea elimu ya juu zaidi, na wanaonekana kuwa na hatima ya kutotimiza ufanisi, matamania yao ya kwanza kabisa katika safari yao ya maisha zilizotowekea tu hewani. Bila kujua kama barabara iliyo mbele ni laini au yenye miamba, wanahisi kwa mara ya kwanza namna ambavyo hatima ya binadamu imejaa vitu vya kubadilikabadilika, na wanachukulia maisha kwa tumaini na hofu. Baadhi ya watu, licha ya kutokuwa na elimu nzuri sana, huandika vitabu na kutimiza kiwango cha umaarufu; baadhi, ingawaje hawajui kusoma na kuandika sana, huunda pesa katika biashara na hivyo basi wanaweza kujikidhi.... Kazi anayochagua mtu, namna mtu anavyozumbua riziki: je, watu wanao udhibiti wowote kuhusu, kama wanaweza kufanya uchaguzi mzuri au uchaguzi mbaya? Je, yanapatana na matamania na uamuzi wao? Watu wengi zaidi hutamani wangeweza kufanya kazi kidogo na kupata mapato mengi zaidi, wasitie bidii sana katika jua na mvua, wavalie vyema, wameremete na kung'aa wakiwa kila pahali, kuwapita sana wengine kwa uwezo, na kuleta heshima kwa mababu zao. Matamania ya watu ni timilifu kweli, lakini watu wanapochukua hatua zao za kwanza katika safari ya maisha yao, wanaanza kwa utaratibu kutambua namna ambavyo hatima ya binadamu ilivyo na hali ya kutokuwa timilifu, na kwa mara ya kwanza wanang'amua kwa kweli hoja hii kwamba, ingawaje mtu anaweza kufanya mipango thabiti kwa minajili ya mustakabali wake, ingawaje mtu anaweza kuhodhi mawazoni ndoto shupavu, hakuna yule aliye na uwezo au nguvu za kutambua ndoto zake mwenyewe, hakuna yule aliye katika hali ya kudhibiti mustakabali wake. Siku zote kutakuwepo na kitalifa fulani kati ya ndoto za mtu na uhalisia ambao lazima mtu akabiliane nao; mambo siku zote hayawi vile ambavyo mtu angetaka yawe, na watu wanapokumbwa na uhalisi kama huu hawawezi kutimiza hali ya kutosheka au kuridhika. Baadhi ya watu wataenda hadi kiwango chochote cha kufikirika, wataweza kutia bidii za kipekee na kujitolea pakubwa kwa minajili ya riziki na mustakabali wao, katika kujaribu kubadilisha hatima yao wenyewe. Lakini hatimaye, hata kama wataweza kutambua ndoto na matamania yao kupitia kwa njia ya bidii yao wenyewe, hawawezi kubadilisha hatima zao, na haijalishi watajaribu vipi kwa njia ya ukaidi hawatawahi kuzidi kile ambacho hatima yao imewapangia. Licha ya tofauti katika uwezo, kiwango cha akili, na hiari ya kutenda, watu wote ni sawa mbele ya hatima, jambo ambalo halileti tofauti kati ya wakubwa na

wadogo, wale wa kiwango kile cha juu na cha chini, wanaotukuzwa na wakatili. Ile kazi ambayo mtu anafuatilia, kile anachofanya mtu ili kuzumbua riziki, na kiwango kipi cha utajiri ambacho mtu amelimbikiza katika maisha yake vyote haviamuliwi na wazazi wa mtu, vipaji vya mtu, jitihada za mtu au malengo ya mtu, vyote vinaamuliwa kabla na Muumba.

2. Kuwaacha Wazazi wa Mtu na Kuanza kwa Bidii Kuendeleza Wajibu Wako Kwenye Ukumbi wa Sanaa wa Maisha

Wakati mtu anapofikia ukomavu, mtu anaweza kuacha wazazi wake na kulikanyaga guu lake nje kivyake, na ni katika wakati huu ambapo mtu huanza kwa kweli kuonyesha wajibu wake binafsi, kwamba kazi maalum ya mtu maishani husita kutoeleweka na polepole kuanza kuwa wazi. Kimsingi mtu huyo bado huonyesha uhusiano wa karibu na wazazi wake, lakini kwa sababu kazi yake maalum na wajibu anaoendeleza katika maisha huwa hauna uhusiano wowote na mama na baba wa mtu huyo, kwa hakika uhusiano huu wa karibu huvunjika polepole kwa kadiri ambavyo mtu anazidi kuendelea kuwa huru. Kutoka katika mtazamo wa kibiolojia, watu bado hawana budi kutegemea wazazi katika njia za kufichika akilini, lakini kama tutaongea kwa malengo, mara baada ya kukua huwa na maisha tofauti kabisa na yale ya wazazi wao, na wataweza kutekeleza wajibu watakaoamua kufanya kwa uhuru wao. Mbali na kuzaliwa na kulea watoto, jukumu la kila mzazi katika maisha ya mtoto ni kuweza kuwapatia tu mazingira rasmi ya kukulia ndani, bila malipo yoyote isipokuwa kule kuamuliwa kabla kwa Muumba ambako kunachukua mwelekeo katika hatima ya mtu huyu husika. Hakuna anayeweza kudhibiti ni mustakabali gani ambao mtu atakuwa nao; huwa umeamuliwa kabla na mapema sana, na hata wazazi wa mtu hawawezi kubadilisha hatima yake. Kulingana na mambo ya hatima, kila mtu yuko huru na kila mtu anayo hatima yake. Kwa hivyo hakuna wazazi wa mtu yeyote wanaweza kuiondoa hatima ya mtu katika maisha au kulisitizia ushawishi wowote ule mdogo katika wajibu ambao mtu huendeleza maishani. Inaweza kusemekana kwamba, familia ambayo mtu ameamuliwa kuzaliwa ndani, na mazingira ambayo mtu atakulia ndani, ni yale masharti ya awali ya kutimiza kazi maalum ya mtu maishani. Yote haya hayaamui kwa vyovyote vile hatima ya mtu katika maisha au aina ya hatima ambayo mtu huyo atatimiza katika kazi yake maalum. Na kwa hivyo hakuna wazazi wa mtu yeyote yule wanaweza kusaidia katika kutimiza kazi hii maalum katika maisha, hakuna watu wowote wa ukoo wanaweza kusaidia mtu kuchukua wajibu huu katika maisha. Vile ambavyo mtu hutimiza kazi yake maalum na katika aina gani ya mazingira ya kuishi ambayo mtu hutekeleza wajibu wake, vyote vinaamuliwa na hatima ya mtu maishani. Kwa maneno mengine, hakuna masharti yoyote mengine yenye malengo yanaweza kuathiri kazi maalum ya mtu, ambayo imeamuliwa kabla na Muumba. Watu wote hukomaa katika mazingira yao binafsi ya kukulia, na kisha kwa taratibu, hatua kwa hatua, huanza safari katika barabara zao binafsi za maisha, hutimiza hatima walizopangiwa na Muumba, kwa

kawaida, bila hiari wao huingia katika bahari kuu ya binadamu na kuchukua nafasi zao binafsi katika maisha, pale ambapo wao huanza kutimiza majukumu yao kama viumbe vilivyoumbwa kwa minajili ya kuamuliwa kabla kwa Muumba, kwa minajili ya ukuu Wake.

Ndoa: Awamu ya Nne

Wakati mtu anavyokua mzee na kukomaa, mtu huanza kukua na kuwa mbali na wazazi wake na mazingira ambayo amezaliwa na kulelewa, na badala yake mtu huanza kutafuta mwelekeo wa maisha yake na kufuatilia shabaha binafsi kwa njia ya maisha iliyo tofauti na ile ya wazazi. Kwenye kipindi hiki cha muda mtu hahitaji tena wazazi wake, bali mwandani ambaye anaweza kuishi maisha yake na mtu huyo: mwenza, mtu ambaye hatima yake imejipinda kwake ndani kwa ndani. Kwa njia hii, tukio kuu ambalo mtu hukabiliana nalo kufuatia uhuru wake ni ndoa, awamu ya nne ambayo lazima mtu apitie.

1. Mtu Hana Chaguo Kuhusu Ndoa

Ndoa ni tukio muhimu katika maisha ya mtu yeyote; ni wakati ule ambao mtu huanza kwa kweli kuendeleza aina mbalimbali za majukumu, huanza kwa utaratibu kutimiza aina mbalimbali za kazi maalum. Watu huwa na picha nyingi kuhusu ndoa kabla ya kuipitia wao wenyewe, na picha hizi zote ni nzuri. Wanawake hufikiria kwamba waume wao watakuwa Kaka Mwenye Mvuto na Haiba, nao wanaume hufikiria kwamba wataweza kuoia Binti wa Kifalme Anayependeza. Kubuni huku kwa mawazo kunaonyesha kwamba kila mtu anayo mahitaji fulani ya ndoa, orodha fulani ya kile anachohitaji na viwango anavyopenda. Ingawaje katika enzi hii ya maovu watu wanaambiwa kila mara kuhusu ujumbe uliopotoka juu ya ndoa, hali ambayo husababisha hata mahitaji mengi zaidi, pamoja na kupatia watu aina zote za mizigo na mitazamo isiyo ya kawaida, mtu yeyote aliyepitia ndoa anajua kwamba haijalishi ni kiasi kipi ambacho mtu ataielewa, haijalishi pia mtu anao mtazamo gani katika ndoa hiyo, ndoa si suala la chaguo la mtu binafsi.

Mtu hukumbana na watu wengi katika maisha yake, lakini hakuna anayejua ni nani atakayekuwa mwandani wake katika ndoa. Ingawaje kila mtu anazo fikira zake binafsi na mtazamo wake wa kibinafsi kuhusu suala la ndoa, hakuna anayeweza kuona mbele na kujua ni nani atakayekuwa mwandani wake wa kweli hatimaye, na fikira za mtu huwa zinachangia kidogo sana. Baada ya kukutana na mtu unayempenda, unaweza kumfuatilia mtu huyo; kama mtu huyo amevutiwa na wewe au la, kama mtu huyo anaweza kuwa mwandani wako au la, si wewe kuamua. Kiini cha mahaba yenu si haswa mtu ambaye mtaweza kuishi naye katika maisha yako; na huku haya yakiendelea mtu ambaye hukuwahi kutarajia anaingia katika maisha yako na kuwa mwandani wako, anakuwa msingi muhimu sana katika hatima yako, nusu yako ile

nyingine, ambaye hatima yako imefungamanishwa naye ajabu. Na kwa hiyo, ingawaje kunazo ndoa milioni kwa milioni ulimwenguni, kila ndoa ni tofauti: Ni ndoa ngapi ambazo hazitoshelezi, ni ngapi zinayo furaha; ni ngapi zinazopatikana Mashariki na Magharibi, ni ngapi Kaskazini na Kusini; ni ngapi ambazo wanandoa wanafaa na wamelingana, na ni ngapi zenye kiwango sawa; ni ngapi zenye furaha na utulivu, ni ngapi zenye maumivu na huzuni; ni ngapi zinaonewa wivu na wengine, na ni ngapi hazieleweki na hazipendelewi kabisa; ni ngapi zimejaa furaha, na ni ngapi zimejaa machozi na zinakatisha tamaa.... Kwenye ndoa hizi zote, binadamu wanafichua utiifu na kujitolea kwa maisha katika ndoa hizo, au pendo, au mtagusano, na hali ya kutotenganishwa, au kukata tamaa na kutoeleweka, au usaliti, au hata chuki. Haijalishi kama ndoa inaleta furaha au maumivu, kazi maalum ya kila mmoja katika ndoa iliamuliwa kabla na Muumba na haitabadilika; kila mmoja lazima aitimize. Na hatima ya kibinafsi inayokuwa katika kila ndoa haibadiliki; iliamuliwa kitambo naye Muumba.

2. Ndoa Inazaliwa Kutokana na Hatima ya Wandani Wote Wawili

Ndoa ni awamu muhimu katika maisha ya mtu. Ni zao la hatima ya mtu, kiungo muhimu katika hatima ya mtu; haiundwi kwa misingi ya uamuzi wa mtu yeyote binafsi au mapendeleo yake, na haiathiriwi na mambo yoyote ya nje, lakini inaamuliwa kabisa na hatima za wandani wawili, kupitia kwa maandalizi na kuamuliwa kabla kwa Muumba kuhusiana na hatima za wanandoa hao. Ukiangalia juujuu, kusudi la ndoa ni kuendeleza kizazi cha binadamu, lakini kwa kweli ndoa si chochote ila ni kawaida ya dini ambayo mtu anapitia katika mchakato wa kutimiza kazi yake maalum. Wajibu mbalimbali ambao watu huendeleza katika ndoa si ule tu wa kuleta kizazi kinachofuata; kunao wajibu mbalimbali ambao mtu huwa nao na kazi maalum ambazo mtu lazima atimize kwenye mkondo wa kuendeleza ndoa. Kwa sababu kuzaliwa kwa mtu huathiri mabadiliko ya watu, matukio, na mambo yanayomzunguka, ndoa ya mtu itaweza pia kuathiri bila shaka watu hao, na zaidi itawabadilisha kwa njia tofauti.

Wakati mtu anapokuwa huru, mtu huanza safari yake binafsi ya maisha, inayoongoza mtu hatua kwa hatua kuelekea kwa watu, na kwa matukio, na kwa vitu vinavyohusiana na ndoa ya mtu; na wakati uo huo, yule mtu mwingine atakayeunda ile ndoa anakaribia, hatua kwa hatua, kuelekea watu hao hao, matukio na hata mambo. Kwenye ukuu wa Muumba, watu wawili wasiohusiana walio na hatima inayohusiana wanaingia kwa utaratibu kwenye ndoa na kuwa, kimiujiza, familia, “nzige wawili wanaoshikilia kamba moja.” Kwa hivyo mtu anapoingia kwenye ndoa, safari ya mtu katika maisha itaathiri na kungusa yule mwenzake, na vilevile safari ya mwandani katika maisha itashawishi na kugusa hatima ya yule mwenzake katika maisha. Kwa maneno mengine, hatima za mwanadamu zimeingiliana na hakuna yule anayeweza kutimiza kazi yake maalum maishani au kutekeleza wajibu wake kabisa akiwa huru mbali na wengine.

Kuzaliwa kwa mtu kunao mwelekeo kwa msururu mkubwa wa mahusiano; kukua pia kunahusisha msururu mkubwa wa mahusiano; na vilevile, ndoa inakuwepo bila shaka na kuendelezwa katika mtandao mpana na mgumu wa miunganisho ya binadamu, ikihusisha kila mwanachama na kuathiri hatima ya kila mmoja ambaye ni sehemu yake. Ndoa si mazao ya familia za wanachama wale wawili, hali ambazo wao walilelewa, maumbo yao, umri wao, ubora wao, vipaji vyao, au mambo mengine yoyote; badala yake, inatokana na kazi maalum ya pamoja na hatima inayohusiana. Hii ndiyo asili ya ndoa, zao la hatima ya binadamu lililopangwa na lililopangiliwa na Muumba.

Uzao: Awamu ya Tano

Baada ya kuoa, mtu ananza kulea kizazi kijacho. Mtu hana uwezo wa kujua atakuwa na watoto wangapi na watoto hawa watakuwa aina gani; hili pia linaamuliwa na hatima ya mtu, iliyoamuliwa kabla na Muumba. Hii ndiyo awamu ya tano ambayo lazima mtu apitie.

Kama mtu amezaliwa ili kutimiza jukumu la mtoto wa mwingine, basi mtu analea kizazi kijacho ili kutimiza jukumu la mzazi wa mwingine. Mabadiliko haya ya majukumu yanamfanya mtu kupitia awamu tofauti za maisha kutoka mitazamo tofauti. Yanampa pia mtu mseto tofauti wa mambo mbalimbali ya maisha kupitia, ambapo mtu anajua ukuu ule wa Muumba, pamoja na hoja kwamba hakuna mtu anayeweza kuzidi au kubadilisha kile ambacho Muumba aliamua kabla.

1. Mtu Hana Udhhibiti wa Hatima ya Uzao Wake

Kuzaliwa, kukua, na kuoa ni awamu ambazo zinaleta aina tofauti na viwango tofauti vya masikitiko. Baadhi ya watu hawatosheki na familia zao au maumbile yao ya kimwili; baadhi hawapendi wazazi wao; baadhi wanachukia au wanalalamikia mazingira ambayo walikulia ndani. Na kwa baadhi ya watu wengi, miongoni mwa masikitiko haya yote, ndoa ndiyo ambayo haitoshelezi zaidi. Licha ya vile ambavyo unayo masikitiko kwa kuzaliwa kwako, au kukua kwako, au ndoa yako, kila mmoja ambaye amepitia awamu hizi amejua kwamba hawezi kuchagua ni wapi au ni lini alizaliwa, ni vipi anavyofanana, wazazi wake ni nani, na mume au mke wake ni nani, lakini wanaweza kukubali tu mapenzi ya Mbinguni. Lakini wakati wa watu kulea kizazi kijacho unapowadia, wataweza kuweka matamano yao yote ambayo hayajitimizwa katika nusu ya kwanza ya maisha yao kwenye vizazi vyao, wakitumai kwamba, uzao wao utajaliza sehemu ile ambayo wao wamepitia masikitiko, kwenye nusu ile ya kwanza ya maisha yao. Kwa hivyo watu hujihusisha katika aina zote za fantasia kuhusu watoto wao: kwamba binti zao watakua na kuwa warembo ajabu, watoto wao wa kiume watakuwa wanaume wa kipekee; kwamba binti zao watakuwa na maadili na wenye vipaji nao watoto wao wa kiume watakuwa

wanafunzi werevu, na wanariadha sifika; na kwamba binti zao watakuwa watulivu na waadilifu, wenye akili razini, kwamba watoto wao wa kiume watakuwa wenye akili, wenye uwezo na wanaojali. Wanatumai kwamba wawe watoto wa kike au wa kiume wataheshimu wazee wao, watajali wazazi wao, watapendwa na kusifiwa na kila mmoja.... Kufikia hapa matumaini ya maisha yanajitokeza upya, na matamania mapya yanapata nguvu katika mioyo ya watu. Watu wanajua kwamba hawana nguvu na tumaini katika maisha haya, kwamba hawatakuwa na fursa nyingine, tumaini jingine, la kujitokeza mbele ya watu, na kwamba hawana chaguo lolote ila kukubali hatima zao. Na kwa hivyo wanatazamia matumaini yao yote, matamania na maadili yao ambayo hayajitimizwa, hadi kwenye kizazi kijacho, wakitumai uzao wao unaweza kuwasaidia kutimiza ndoto zao na kutambua matamania yao; na kwamba binti zao na watoto wao wa kiume wataleta utukufu katika jina la familia, kuwa muhimu, kuwa matajiri au maarufu; kwa ufupi, wanataka kuuona utajiri wa watoto wao ukizidi na kuzidi. Mipango na fantasia za watu ni timilifu; kwani hawajui kwamba idadi ya watoto walio nayo, umbo, uwezo na kadhalika wa watoto wao, si juu yao kuamua, kwamba hatima za watoto wao hazimo kamwe katika viganja vya mikono yao? Binadamu si waendeshaji wa hatima yao binafsi, ilhali wanatumai kubadilisha hatima ya kizazi kichanga zaidi; hawana nguvu za kutoroka hatima zao wenyewe, ilhali, wanajaribu kudhibiti zile za watoto wao wa kiume na kike. Je, hawazidishi ukadiriaji wao? Je, huu si ujinga na hali ya kutojua kwa upande wa binadamu? Watu huenda kwa mapana yoyote kwa minajili ya uzao wao, lakini hatimaye, idadi ya watoto aliyonayo mtu, na vile ambavyo watoto wake walivyo, si jibu la mipango na matamania yao. Baadhi ya watu hawana hela lakini wanazaa watoto wengi; baadhi ya watu ni tajiri ilhali hawana mtoto. Baadhi wanataka binti lakini wananyimwa tamania hilo; baadhi wanataka mtoto wa kiume lakini wanashindwa kuzaa mtoto wa kiume. Kwa baadhi, watoto ni baraka; kwa wengine, mtoto ni laana. Baadhi ya wanandoa ni werevu, ilhali wanawazaa watoto wanaoelewa polepole; baadhi ya wazazi ni wenye bidii na waaminifu, ilhali watoto wanaowalea ni wavivu. Baadhi ya wazazi ni wapole na wanyofu lakini wana watoto wanaogeuka na kuwa wajanja na wenye inda. Baadhi ya wazazi wana akili na mwili timamu lakini wanajifungua watoto walemavu. Baadhi ya wazazi ni wa kawaida na hawajafanikiwa ilhali watoto wao wanafanikiwa pakubwa. Baadhi ya wazazi ni wa hadhi ya chini ilhali watoto wanaowalea ni wenye taadhima. ...

2. Baada ya Kulea Kizazi Kijacho, Watu Hufaidi Ufahamu Mpya wa Hatima Yao

Watu wengi wanaooa hufanya hivyo karibu kwenye umri wa miaka thelathini, na kwa wakati huu wa maisha, mtu hana ufahamu wowote wa hatima ya binadamu. Lakini wakati watu wanapoanza kulea watoto, kwa kadri uzao wao unapokua, wanatazama kizazi kipya kikirudia maisha na hali zote walizopitia katika kizazi cha awali, na wanaona maisha yao ya kale yakijionyesha kwao na wanatambua kwamba barabara inayotumiwa na kizazi kile kichanga

zaidi, kama tu yao, haiwezi kupangwa wala kuchaguliwa. Wakiwa wamekabiliwa na hoja hii, hawana chaguo lolote bali kukubali kwamba hatima ya kila mtu iliamuliwa kabla; na bila ya hata kutambua wanaanza kwa utaratibu kuweka pembeni matamania yao binafsi, na hisia kali katika mioyo yao inapungua na kuwatoka.... Kwenye kipindi hiki cha muda, mtu ameweza kupita sehemu nyingi zaidi na muhimu katika mafanikio ya maisha yake na ametimiza ufahamu mpya wa maisha, na kuchukua mtazamo mpya. Je, mtu wa umri huu anaweza kutarajia kwa siku za usoni kiasi kipi cha mambo na ni matarajio yapi wanayotazamia? Ni mwanamke yupi mwenye umri wa miaka hamsini angali anaota kuhusu Kaka Mwenye Mvuto na Haiba? Ni mwanamume yupi wa miaka hamsini angali anatafuta Binti wa Kifalme Anayependeza? Ni mwanamke yupi wa umri wa kati atakuwa anatumai kugeuka kutoka kwa mtoto wa bata mwenye sura mbaya hadi batamaji? Je, wanaume wazee zaidi wangali wana msukumo sawa wa ajira na wanaume wachanga? Kwa ujumla, haijalishi kama mtu ni mwanamume au mwanamke, yeyote anayeishi na kuufikia umri huu anao uwezekano wa kuwa na mtazamo wa kueleweka na kutumika kiasi fulani katika ndoa, familia, na watoto. Mtu kama huyo, kimsingi hana chaguo zozote zilizobakia, hana msukumo wowote wa kukabiliana na hatima yake. Kwa mujibu wa kile ambacho binadamu amepitia, punde tu mtu anapofikia umri huu mtu huanza kwa kawaida kuwa na mtazamo kwamba “lazima mtu akubali hatima yake; watoto wake wanao utajiri wao binafsi; hatima ya binadamu inaanamriwa Mbinguni.” Watu wengi ambao hawaelewi ukweli, baada ya kupitia mabadiliko, mahangaiko, na ugumu wote wa ulimwengu huu, watatoa muhtasari wa utambuzi wao wa maisha ya binadamu kwa maneno matatu: “Hiyo ndiyo hatima!” Ingawaje kauli hii inatoa muhtasari wa hitimisho ya watu wa ulimwengu na utambuzi kuhusu hatima ya binadamu, ingawaje inaelezea kutoweza kusaidika kwa binadamu na inaweza kusemekana kwamba inapenyeza na ni sahihi, ni kilio cha mbali kutoka kwa ufahamu wa ukuu wa Muumba, na si kibadala cha maarifa ya mamlaka ya Muumba.

3. Kusadiki Katika Hatima si Mbadala wa Maarifa ya Ukuu wa Muumba

Baada ya kuwa mfuasi wa Mungu kwa miaka mingi, je, kunayo tofauti kubwa katika maarifa yenu ya hatima na yale ya watu wa ulimwengu? Je, mmeelewa kwa kweli kule kuamuliwa kabla kwa Muumba, na unaweza kujua kwa kweli ukuu wa Muumba? Baadhi ya watu wanao ufahamu mkuu, wa kina wa kauli hii “hiyo ndiyo hatima,” ilhali hawasadiki hata kidogo katika ukuu wa Mungu, hawasadiki kwamba hatima ya binadamu hupangiliwa na kupangwa na Mungu, na hawako radhi kunyenyekea mbele ya ukuu wa Mungu. Watu kama hao ni kana kwamba wanaelea baharini, wanatoswatoswa na mawimbi, huku wakielea na kufuata mkondo wa maji, wasiwe na chaguo ila kusubiri kimyakimya na kuachia maisha yao hatima. Ilhali hawatambui hatima ya binadamu inategemea ukuu wa Mungu; hawawezi kujua ukuu wa Mungu wao binafsi, na hivyo basi kutimiza utambulisho wa mamlaka ya Mungu, kunyenyekea

katika mipango na mipangilio ya Mungu, kuacha kukinzana na hatima na kuishi katika utunzwaji, ulinzi na mwongozo wa Mungu. Kwa maneno mengine, kukubali hatima si jambo sawa na kunyenyekea kwa ukuu wa Muumba; kusadiki hatima hakumaanishi kwamba mtu akubali, atambue, na ajue ukuu wa Muumba; kusadiki katika hatima ni ule utambulisho wa hoja hii na suala hili la nje, ambalo ni tofauti na kujua namna Muumba Anavyotawala hatima ya binadamu, kuanzia katika kutambua kwamba Muumba ndiye chanzo cha kutawala juu ya hatima za mambo yote na hata zaidi kunyenyekea kwa mipango na mipangilio ya Muumba kwa ajili ya hatima ya binadamu. Kama mtu anasadiki tu katika hatima—hata anahisi kwa kina kuihusu—lakini papo hapo hawezi kujua, kutambua, kunyenyekea, na kukubali ukuu wa Muumba kuhusu ile hatima ya binadamu basi maisha yake yatakuwa kwa kweli msiba mkuu, maisha yaliyopita kwa masikitiko, utupu; yeye atakuwa hawezi kutii utawala wa Muumba, kuwa binadamu aliyeumbwa katika hali ya kweli zaidi ya kauli hiyo, na kufurahia idhini ya Muumba. Mtu anayejua na kupitia kwa kweli ukuu wa Muumba anafaa kuwa katika hali amilifu, isiyo baridi au ya kutoweza kusaidika. Huku wakati uo huo akikubali kwamba mambo yote yanategemea hatima ya maisha, yeye anafaa kumiliki ufafanuzi sahihi wa maisha na hatima: kwamba kila maisha yanategemea ukuu wa Muumba. Wakati mtu anapoangalia nyuma kwenye barabara aliyotembelea, wakati mtu anapokusanya tena kila awamu ya safari ya maisha yake, mtu anaona kila hatua, haijalishi kama barabara ya mtu inakuwa mbaya au nzuri, Mungu alikuwa akiongoza njia ya mtu, akipanga kila kitu. Ilikuwa ni mipangilio ya umakinifu ya Mungu, upangiliaji Wake makinifu ulioongoza mtu, bila kujua, hadi kufikia leo. Ili kuweza kukubali ukuu wa Muumba, ili kupokea wokovu Wake—utajiri mwingi kweli! Kama mtazamo wa mtu katika hatima ni wa baridi, inathibitisha kwamba yeye anakinzana na kila kitu ambacho Mungu amepangilia, kwamba yeye hana mtazamo wa kunyenyekea. Kama mtazamo wa mtu katika ukuu wa Mungu juu ya hatima ya binadamu ni amilifu, basi mtu anapotazama nyuma katika safari yake, wakati mtu anapong'amua kwa kweli ukuu wa Mungu, mtu huyo ataweza kutamani kwa dhati kunyenyekea kila kitu ambacho Mungu amepangilia, atakuwa na jitihada zaidi na ujasiri wa kumwacha Mungu kuunda hatima yake, ili kuacha kuasi dhidi ya Mungu. Kwani mtu anaona kwamba akikosa kuelewa hatima, wakati mtu haelewi ukuu wa Mungu, wakati mtu anapotutusa mbele kwa hiari yake, akichechemea na kupenyeza kwenye ukungu, safari inakuwa ngumu sana, ya kuvunja moyo. Kwa hivyo wakati watu wanapotambua ukuu wa Mungu juu ya hatima ya binadamu, wale walio werevu wanachagua kuijua na kuikubali, kuaga kwaheri siku zenye maumivu ambapo walijaribu kuwa na maisha mazuri kwa nguvu za mikono yao miwili, badala ya kuendelea kung'ang'ana dhidi ya hatima na kuzitafuta zile shabaha maarufu za maisha kwa njia yao wenyewe. Wakati mtu hana Mungu, wakati mtu hawezi kumwona Mungu, wakati hawezi kutambua waziwazi ukuu wa Mungu, kila siku inakosa maana, inakosa thamani, na kuwa yenye taabu. Popote pale mtu yupo, kazi yoyote ile anayofanya, mbinu za mtu za kuzumbua

riziki na kutafuta shabaha zake huweza kumletea kitu kimoja ambacho ni kuvunjika moyo kusikoisha na mateso yasiyopona, kiasi cha kwamba mtu hawezi kuvumilia kuangalia nyuma. Ni pale tu mtu anapokubali ukuu wa Muumba, ananyenyekea katika mipango na mipangilio Yake, na kutafuta maisha ya kweli ya binadamu, ndipo mtu atakapokuwa huru kwa utaratibu dhidi ya kuvunjika moyo na kuteseka, kutupilia mbali utupu wote wa maisha.

4. Wale tu Wanaonyenyekea Ukuu wa Muumba Ndio Wanaweza Kupata Uhuru wa Kweli

Kwa sababu watu hawatambui mipango ya Mungu, na ukuu wa Mungu, siku zote wanakabiliana na hatima hiyo kwa kuasi, kwa mtazamo wa kuasi, na siku zote wanataka kutupilia mbali mamlaka na ukuu wa Mungu, na mambo yale ambayo hatima imewahifadhia, wakitumai kwamba watabadilisha hali zao za sasa na kubadilisha hatima yao. Lakini hawawezi kufaulu; wanazuiliwa kwa kila sehemu ya mabadiliko katika maisha. Mvutano huu, unaoendelea ndani ya nafsi ya mtu, ni wa maumivu; maumivu haya hayasahauliki; na wakati wote huu mtu anapoteza maisha yake mwenyewe. Sababu ya maumivu haya ni nini? Je, ni kwa sababu ya ukuu wa Mungu au kwa sababu ya mtu kuzaliwa bila bahati? Bila shaka kati ya sababu hizi hakuna iliyo kweli. Kimsingi, ni kwa sababu ya njia ambazo watu huchukua, njia ambazo watu huchagua kuishi katika maisha yao. Baadhi ya watu huenda wasitambue mambo haya. Lakini unapojua kwa kweli, unapotambua kwa kweli kwamba Mungu anao ukuu juu ya hatima ya binadamu, unapoelewa kwa kweli kwamba kila kitu ambacho Mungu amekupangilia na kukuamulia ni chenye manufaa makubwa, na ni ulinzi mkubwa, basi unahisi maumivu yako yakipungua kwa utaratibu, na uzima wako wote unaanza kutulia, kuwa huru na kukombolewa. Tukiamua kutokana na hali za wingi wa watu, ingawaje kwa kiwango cha kibinafsi hawataki kuendelea kuishi kama walivyokuwa wakiishi awali, ingawaje wanataka tulizo katika maumivu yao, kimsingi hawawezi kung'amua kwa kweli thamani na maana halisi ya ukuu wa Muumba ya hatima ya binadamu; hawawezi kutambua kwa kweli na kunyenyekea kwa ukuu wa Muumba, isitoshe kujua namna ya kutafuta na kukubali mipango na mipangilio ya Muumba. Kwa hivyo kama watu hawawezi kutambua hoja kwamba Muumba anao ukuu juu ya hatima ya binadamu na juu ya mambo yote ya binadamu, kama hawawezi kunyenyekea kwa kweli chini ya utawala wa Muumba, basi itakuwa vigumu sana kwao kutoendeshwa na kutiwa pingu za miguu na, fikira hii kwamba “hatima ya mtu imo kwenye mikono ya mtu,” itakuwa vigumu kwao kutupilia mbali maumivu ya kung'ang'ana kwao kwingi dhidi ya hatima na mamlaka ya Muumba, ni wazi kwamba hali hii pia itakuwa ngumu kwao katika kuweza kukombolewa kwa kweli na kuwa huru, kuwa watu wanaoabudu Mungu. Kunayo njia rahisi zaidi ile ya kujifanya kuwa huru kutoka katika hali hii: kuaga kwaheri njia yako ya awali ya kuishi, kuaga kwaheri shabaha zako za maisha za awali, kuhitimisha na kuchambua hali ya maisha ya awali, mtazamo wa maisha, mambo uliyofuatilia, matamania, na maadili, na kisha kuyalinganisha yote haya na mapenzi ya

Mungu na mahitaji ya binadamu, na kuona kama yoyote kati ya haya yanakubaliana na mapenzi na mahitaji ya Mungu, kujua kama yoyote kati ya haya yanakuletea maadili sahihi ya maisha, yanakuongoza katika ufahamu mwingi zaidi wa ukweli, na kuruhusu mtu kuishi kwa ubinadamu na mfano wa binadamu. Unapochunguza mara kwa mara na kuchambua kwa makini shabaha mbalimbali za maisha ambazo watu hufuatilia na njia zao tofauti za kuishi, utapata kwamba hata hakuna moja kati ya hizo zote ambayo inaingiliana na nia ya Muumba wakati Alipoumba binadamu. Zote hizi zinawavuta watu mbali na ukuu na utunzwaji wa Muumba; zote ni mitego ambayo huwasababisha watu wawe wapotovu, na ambayo inawaelekeza jehnamu. Baada ya kutambua haya, kazi yako ni kuweka pembeni mtazamo wako wa maisha ya awali, kuwa mbali na mitego mbalimbali, kumwachia Mungu kuchukua usukani wa maisha yako na kukufanyia mipangilio, jaribu tu kunyenyekea katika mipango na mwongozo wa Mungu, kutokuwa na chaguo, na kuwa mtu anayemwabudu Mungu. Haya yote yanaonekana kuwa rahisi, lakini ni jambo gumu kufanya. Baadhi ya watu wanaweza kuvumilia maumivu yake, wengine hawawezi. Baadhi wako radhi kutii, wengine hawako radhi. Wale wasiokuwa radhi wanakosa tamanio na uamuzi wa kufanya hivyo; wanayo habari kamili kuhusu ukuu wa Mungu, wanajua vyema kabisa kwamba ni Mungu anayepangilia na kupanga hatima ya binadamu, na ilhali wangali wanang'ang'ana tu, bado hawajaridhiana na nafsi zao kuhusiana na kuziacha hatima zao kwenye kiganja cha mkono wa Mungu na kunyenyekea katika ukuu wa Mungu, na zaidi, wanachukia mipango na mipangilio ya Mungu. Kwa hivyo, siku zote kutakuwa na baadhi ya watu wanaotaka kujionea wenyewe kile wanachoweza kufanya; wanataka kubadilisha hatima zao wenyewe kwa mikono yao miwili, au kutimiza furaha kwa kutumia nguvu zao wenyewe, kuona kama wanaweza kukiuka mipaka ya mamlaka ya Mungu na kuinuka juu ya ukuu wa Mungu. Huzuni ya binadamu, si kwamba binadamu anatafuta maisha mazuri, si kwamba anatafuta umaarufu na utajiri au anang'ang'ana dhidi ya hatima yake mwenyewe kupitia kwenye ukungu, lakini kwamba baada ya yeye kuona uwepo wa Muumba, baada ya yeye kujifunza hoja kwamba Muumba anao ukuu juu ya hatima ya binadamu, bado hawezi kurekebisha njia zake, hawezi kuvuta miguu yake kutoka kwenye mtego, lakini anaufanya moyo wake kuwa mgumu na anasisitizia makosa yake. Afadhali aendeleo kutapatapa kwenye matope, akiapa kwa ukaidi dhidi ya ukuu wa Muumba, akiupinga mpaka mwisho wake mchungu, bila ya hata chembechembe kidogo ya majuto, na mpaka pale anapolazwa akiwa amevunjika na anavuja damu ndipo anapoamua hatimaye kusalimu amri na kugeuka na kubadilisha mwenendo. Kwa kweli huu ni huzuni kwa binadamu. Kwa hivyo Ninasema, wale wanaochagua kunyenyekea ni werevu na wale waliochagua kutoroka ni vichwa vigumu.

Kifo: Awamu ya Sita

Baada ya mahangaiko mengi na masikitiko mengi, na kuvunjwa moyo kwingi, baada ya

furaha nyingi na huzuni nyingi na baada ya misukosuko ya maisha, baada ya miaka mingi sana isiyosahaulika, baada ya kutazama misimu ikipita na kujirudia, mtu hupita kwenye kiungo muhimu sana cha maisha bila ya taarifa, na kwa ghafla tu mtu anajipata kwenye miaka yake ya kufifia. Alama za muda zimejichora kotekote kwenye mwili wa mtu: Mtu hawezi tena kusimama wima, kichwa cha nywele nyeusi kinageuka na kuwa cha nywele nyeupe, macho maangavu na mazuri yanabadilika na kuanza kufifiliza na kuwa na wingu mbele yao, nayo ngozi laini, yenye unyumbufu inageuka na kuwa na makunyanzi na madoadoa. Kusikia kwa mtu kunaanza kufifia, meno yake kulegea na kuanza kujiangukia, mwitikio wa mtu unaanza kuchelewachelewa, kutembea kunakuwa ni kwa kujikokota.... Wakati huu mtu ameaga kwaheri kabisa miaka yake ya nguvu ya ujana wake na kuingia katika maisha yake ya kwaheri: umri wa uzee. Kisha, mtu atakabiliana na kifo, awamu ya mwisho ya maisha ya binadamu.

1. Muumba Pekee Ndiye Anayeshikilia Nguvu za Maisha na Kifo juu ya Binadamu

Kama kuzaliwa kwa mtu kulipangiwa na maisha ya awali ya mtu, basi kifo cha mtu kinaadhimisha mwisho wa hatima hiyo. Kama kuzaliwa kwa mtu ndiyo mwanzo wa kazi maalum ya mtu ya maisha, basi kifo cha mtu kinaadhimisha mwisho wa kazi hiyo maalum. Kwa sababu Muumba amepangilia mseto maalum wa hali mbalimbali za kuzaliwa kwa mtu, ni wazi na dhahiri shahiri kwamba amepangilia pia mseto wa hali zisizobadilika kwa minajili ya kifo cha mtu. Kwa maneno mengine, hakuna anayezaliwa kwa bahati na hakuna kifo cha mtu ambacho hakitarajiwi, na si kuzaliwa, si kufa vyote vina uhusiano na maisha ya mtu ya awali na ya sasa. Hali za kuzaliwa na kifo cha mtu, vyote viliamuliwa kabla na Muumba; hii ni kudura ya mtu, hatima ya mtu. Kama vile tu mengi yanaweza kuzungumzwa kuhusu kuzaliwa kwa mtu, hata kifo cha kila mtu kitafanyika katika mseto tofauti katika hali maalum, hivyo basi urefu wa maisha tofauti miongoni mwa watu na njia tofauti pamoja na nyakati tofauti zinaandama vifo vyao. Baadhi ya watu wana nguvu na afya na ilhali wanakufa mapema; wengine ni wanyonge na wanauguaugua ilhali wanaishi hadi umri wa uzee, na wanaaga dunia kwa amani. Baadhi wanafarakana na dunia kutokana na sababu zisizokuwa za kawaida, wengine kutokana na sababu za kawaida. Baadhi wanakata roho wakiwa mbali na nyumbani, wengine wanayafumba macho yao kwa mara ya mwisho wakiwa na wapendwa wao kando yao. Baadhi ya watu hufia hewani, wengine hufia chini ya nchi. Wengine huzama chini ya maji, wengine nao kwenye majanga. Baadhi hufa asubuhi, wengine hufa usiku. ... Kila mtu hutaka kuzaliwa kwa heshima, maisha mazuri, na kifo kitukufu, hakuna mtu anayeweza kufika zaidi ya hatima yake mwenyewe, hakuna mtu anayeweza kukwepa ukuu wa Muumba. Hii ni hatima ya binadamu. Binadamu anaweza kufanya aina zote za mipango ya siku zote za usoni, lakini hakuna mtu anayeweza kupanga njia na muda wa kuzaliwa kwake na kuondoka kwake ulimwenguni. Ingawaje watu hufanya kila wawezalo kuepuka na kuzuia kuja kwa kifo chao, ilhali, bila wao kujua, kifo huwa

kinakaribia polepole. Hakuna anayejua ni lini atakapofarakana na dunia au ni vipi, isitoshe hata pale hayo yote yatakapofanyikia. Bila shaka, si binadamu wanaoshikilia nguvu za maisha na kifo, wala si kiumbe fulani kwenye ulimwengu wa kimaumbile, lakini ni Muumba, ambaye mamlaka yake ni ya kipekee. Maisha na kifo cha binadamu si zao la sheria fulani ya ulimwengu wa kimaumbile, lakini athari ya ukuu wa mamlaka ya Muumba.

2. Yule Asijejua Ukuu wa Muumba Atahangaika kwa Woga wa Kifo

Wakati mtu anapoingia kwenye umri wa uzee, changamoto anazokabiliana nazo si kutosheleza mahitaji ya familia au kuanzisha maono makubwa katika maisha yake, lakini namna ya kuyaaga maisha yake, namna ya kukutana na mwisho wa maisha yake, namna ya kuweka kikomo kwenye mwisho wa uwepo wake binafsi. Ingawaje juujuu inaonekana kwamba watu hutilia makini kidogo kwa kifo, hakuna anayeweza kuepuka kuchunguza suala hili, kwani hakuna anayejua ikiwa ulimwengu mwingine uko kule upande mwingine wa kifo, ulimwengu ambao binadamu hawawezi kung'amua au kuhisi, ulimwengu wasiojua chochote kuhusu. Hali hii huwafanya watu kuwa na wasiwasi kukabiliana na kifo moja kwa moja, wasiwasi wa kukabiliana nacho kama inavyostahili, na badala yake wanafanya kadri ya uwezo wao kuepuka mada hii. Na kwa hivyo mada hii humfanya kila mmoja kutishika kuhusu kifo, huongezea uzito kwenye fumbo hili kuhusiana na hoja hii isiyokwepeka ya maisha, huweka kivuli kisichoisha juu ya moyo wa kila mmoja.

Wakati mtu anapohisi mwili wake unaanza kudhoofika, wakati mtu anapohisi kwamba kifo chake chakaribia, mtu huhisi tishio, woga usioelezeka. Woga wa kifo humfanya mtu kuhisi kuwa mpweke zaidi na asiyejiweza, na kwa wakati huu mtu hujiuliza: Nilitoka wapi? Ninaenda wapi? Je, hivi ndivyo nitakavyokufa, huku maisha yangu yakinipita kwa haraka hivi? Je, huu ndio wakati unaoadhimisha mwisho wa maisha yangu? Ni nini, hatimaye, maana ya maisha? Maisha yana thamani gani, kwa kweli? Je, yanahusu umaarufu na utajiri? Je, yanahusu kulea familia? ... Haijalishi kama mtu amewahi kufikiria maswali haya mahususi, haijalishi ni vipi mtu ana woga wa kifo, katika kina cha moyo wa kila mmoja siku zote kuna tamani la kutaka kuchunguza zaidi mafumbo, hisia zisizoeleweka kuhusu maisha, pamoja na haya yote, ni uhusiano wa karibu na ulimwengu wenyewe, na kutotaka kuuacha. Pengine hakuna anayeweza kufafanua zaidi ni nini ambacho binadamu huogopa, ni nini ambacho binadamu hutaka kuchunguza zaidi, na nini kile ambacho ana uhusiano wa karibu nacho na kinachomfanya kutotaka kuondoka au kukiacha nyuma ...

Kwa sababu wanaogopa kifo, watu huwa na wasiwasi mno; kwa vile wanaogopa kifo, vipo vitu vingi ambavyo hawawezi kuachilia. Wakati wako karibu kufa, baadhi ya watu huhangaika kuhusu hiki au kile; wanakuwa na wasiwasi kuhusu watoto wao, wapendwa wao, utajiri wao, ni

kana kwamba kwa kuwa na wasiwasi hivyo wanaweza kuondoa mateso na hofu ambayo kifo huleta, ni kana kwamba kwa kuendeleza aina fulani ya urafiki wa karibu na wale wanaoishi wanaweza kukwepa ile hali ya kutoweza kujisaidia na upweke unaoandamana na kifo. Katika kina cha moyo wa binadamu kuna woga usiokamilika, woga wa kuachwa na wapendwa, woga wa kutowahi kutuliza macho yako kwenye mbingu za samawati, woga wa kutowahi tena kuangalia ulimwengu huu yakinifu. Nafsi pweke, iliyozeana na wapendwa wake, husita kuachilia mshiko wa maisha na kuondoka, ikiwa pekee, kuelekea kwenye ulimwengu usiojulikana, usiozeleka.

3. Maisha ya Kuishi Ukitafula Umaarufu na Utajiri Yatamwacha Mtu Akiwa na Hasara Akikabiliwa na Kifo

Kwa sababu ya ukuu na kuamuliwa kabla kwa Muumba, nafsi pweke iliyoanza bila chochote kwa jina lake huweza kupata wazazi na familia, fursa ya kuwa mwanachama wa kizazi cha binadamu, fursa ya kupitia maisha ya binadamu na kuona ulimwengu; na pia inafaidi fursa ya kupitia ukuu wa Muumba, kujua uzuri wa uumbaji wa Muumba, na zaidi kuliko vyote, kujua na kutii mamlaka ya Muumba. Lakini watu wengi zaidi huwa hawatumii vizuri fursa hii nadra na ya kipekee. Mtu hutumia nguvu zake zote maishani akipigana dhidi ya hatima yake, akatumia muda wake wote akihangaika na akijaribu kulisha familia yake na akisafiri huku na kule kati ya kutafuta utajiri na hadhi katika jamii. Mambo ambayo watu huthamini ni familia, pesa, na umaarufu; wanaona mambo haya kuwa mambo yenye thamani zaidi katika maisha. Kila mtu hulalamikia hatima yake, ilhali bado wanazisukuma hatima hizi nyuma ya akili zao na wanabaki na maswali ambayo ni lazima zaidi kuchunguza na kuelewa: kwa nini binadamu yuko hai, namna ambavyo binadamu anafaa kuishi, ni nini maana na thamani ya maisha. Katika maisha yao yote, hata hivyo iwe miaka mingapi, wanakimbilia tu kuhusu kutafuta umaarufu na utajiri, mpaka ujana wao ukawaacha, mpaka wakawa na nywele za kijivu na makunyanzi kwenye uso wao; mpaka wakagundua utajiri na umaarufu ni vitu visivyoweza kusitisha mtu kuelekea katika udhaifu unaotokana na uzee, kwamba pesa haiwezi kujaza utupu wa moyo: mpaka wanapoelewa kwamba hakuna mtu ambaye anaachwa nje kutoka kwenye sheria ya kuzaliwa, kuwa mzee, magonjwa, na kifo, kwamba hakuna mtu anayeweza kutoroka hatima ile inayomsabiri. Mpaka tu pale ambapo anapolazimishwa kukabiliwa na awamu ya mwisho maishani ndipo anapong'amua kwa kweli kwamba hata kama mtu anamiliki mamilioni ya mali, hata kama mtu anayo heshima na cheo kikubwa, hakuna anayeweza kutoroka kifo, kwamba kila mtu atarudi kwenye sehemu yake asilia: nafsi pweke, bila chochote kwa jina lake. Wakati mtu anapokuwa na wazazi, mtu husadiki kwamba wazazi wa mtu ni kila kitu; wakati mtu anapokuwa na mali, mtu hufikiri kwamba pesa ndizo kitu cha muhimu, kwamba ndizo namna ambayo kwayo mtu huishi; wakati watu wanapokuwa na hadhi katika jamii, wanaishikilia na hata wanaweza kuhatarisha maisha

yao kwa ajili ya hadhi hiyo. Ni pale tu ambapo watu wanakaribia kuondoka ulimwenguni ndipo wanapotambua kwamba mambo yale waliyoishi katika maisha yao wakifuatilia si chochote bali mawingu yanayopita, hakuna chochote kati ya vitu hivi ambacho wanaweza kushikilia, hakuna hata chochote wanachoweza kwenda nacho, hakuna hata chochote kinachoweza kuwaondolea kifo, hakuna kile kinachoweza kuwapa ushirika au tulizo wakati nafsi yao inapokuwa pweke ikielekea kufa; na hata, hakuna kati ya hivyo vyote vinavyoweza kumpa mtu wokovu, na kuwaruhusu kushinda kifo. Umaarufu na utajiri ambao mtu hupata kwenye ulimwengu yakinifu humpa mtu kutosheka kwa muda, anasa ya kupita, hisia ya uwongo ya utulivu, na kumfanya mtu kupoteza njia. Na kwa hivyo watu, wanapong'ang'ana kila pahali kwenye bahari pana ya binadamu, wakitafuta amani, tulizo na utulivu wa moyo, wanafunikwa zaidi na zaidi na mawimbi. Wakati ambapo watu hawajapata maswali ambayo ni muhimu zaidi kuelewa—ni wapi wametoka, ni kwa nini wako hai, ni wapi wanakoenda na kadhalika—wanashawishiwa na umaarufu na utajiri, wanapotoshwa, wanadhibitiwa na vitu hivyo, na wanaishia kupotea bila kujua njia. Muda huyoyoma; miaka hupita kama kupepeswa kwa jicho; kabla ya mtu kutambua, mtu huaga kwaheri miaka yake bora zaidi ya maisha yake. Wakati mtu anakaribia kuondoka ulimwenguni, mtu anafika katika utambuzi wa taratibu kwamba kila kitu ulimwenguni kinamwacha polepole, kwamba mtu hawezi kushikilia tena vitu alivyomiliki; kisha mtu anahisi kwa kweli kwamba hamiliki chochote kamwe, kama mtoto mchanga anayelia ambaye ndio mwanzo amezaliwa na kubisha mlango ulimwenguni. Wakati huu, mtu anashawishiwa kutafakari kile ambacho amefanya maishani, thamani ya kuwa hai, ni nini maana yake, kwa nini mtu alikuja ulimwenguni; na wakati huu, mtu anaendelea kutaka kujua kama kweli kunayo maisha ya baadaye, kama Mbinguni kweli ipo, kama kweli kunayo adhabu.... Kwa kadri mtu anavyokaribia kifo, ndipo anavyotaka zaidi kuelewa maisha yanahusu nini haswa; kwa kadri mtu anavyokaribia kifo, ndipo moyo wake unapoonekana kuwa mtupu; kwa kadri mtu anavyokaribia kifo, ndipo anapohisi kuwa hawezi kusaidika; na kwa hivyo woga wa mtu kuhusu kifo unazidi kuwa mwingi siku baada ya siku. Kunazo sababu mbili zinazoelezea kwa nini watu huwa hivi wanapokaribia kifo: Kwanza, wako karibu kupoteza umaarufu na utajiri ambao maisha yao yalitegemea, wako karibu kuacha nyuma kila kitu kinachoonekana ulimwenguni; na pili, wako karibu kukabiliana, wakiwa peke yao, na ulimwengu usiojulikana, wenye mafumbo, himaya isiyojulikana ambapo wana woga wa kukanyaga guu lao kule, kule wasikokuwa na wapendwa na mbinu zozote za kupata msaada. Kwa hizo sababu mbili, kila mmoja anayekabiliana na kifo huhisi vibaya, hupitia hali ya wasiwasi na hujipata katika hali ya kutoweza kusaidika ambayo hawajawahi kupitia awali. Kwa hakika punde watu wanapofikia wakati huu ndipo wanapotambua kwamba kitu cha kwanza ambacho mtu lazima aelewe, anapokanyaga guu lake hapa duniani, ni wapi binadamu hutoka, kwa nini watu wako hai, nani anayeamuru hatima ya binadamu, ni nani anayekidhi mahitaji ya binadamu, na Aliye na ukuu juu ya uwepo wa

binadamu. Maarifa haya ndiyo njia ya kweli ambayo kwayo mtu huishi, msingi muhimu kwa kuwepo kwa binadamu—kutojifunza namna ya kutosheleza familia ya mtu au namna ya kutimiza umaarufu na utajiri, kutojifunza namna ya kujitokeza katika umati wala namna ya kuishi maisha mazuri zaidi, bila kutaja namna ya kutia fora na kushindana kwa ufanisi dhidi ya wengine. Ingawaje mbinu mbalimbali za kuishi ambazo watu huishi wakijaribu kumiliki zinaweza kumpa wingi wa tulizo la mali, hazijawahi kuleta amani na tulizo la kweli moyoni, lakini badala yake hufanya watu kila wakati kupoteza mwelekeo wao, kuwa na wakati mgumu kujidhibiti, na kukosa kila fursa ya kujifunza maana ya maisha; mbinu hizi za kuishi huleta mawimbi fiche ya wasiwasi kuhusu namna ya kukabiliana na kifo vizuri. Maisha ya watu huharibika kwa njia hii. Muumba hushughulikia kila mmoja bila mapendeleo, huku akipatia kila mmoja wetu fursa ya kutosha maisha yote ili kuweza kupitia na kujua ukuu Wake, ilhali ni mpaka tu kifo kinapokaribia, wakati kivuli cha kifo kinaponing'inia karibu na mtu, ndipo mtu huyu huanza kuona nuru—na kisha muda huwa umeyoyoma mno.

Watu huishi maisha yao wakitafuta pesa na umaarufu; wanashikilia nyuzi hizi, wakifikiri kwamba ndizo mbinu zao pekee za msaada, ni kana kwamba wakiwa nazo wangeendelea kuishi, wangejitoa kwenye hesabu ya wale watakaokufa. Lakini pale tu wanapokuwa karibu kufa ndipo wanapotambua namna ambavyo vitu hivi vilivyo mbali na wao, namna walivyo wanyonge mbele ya kifo, namna wanavyosambaratika kwa urahisi, namna walivyo wapweke na wasivyoweza kusaidika, na hawana popote pa kugeukia. Wanatambua kwamba maisha hayawezi kununuliwa kwa pesa au umaarufu, kwamba haijalishi mtu ni tajiri vipi, haijalishi cheo chake kilivyo cha hadhi, watu wote ni maskini kwa njia sawa na wanaofanya mambo bila mpango mbele ya kifo. Wanatambua kwamba pesa haiwezi kununua maisha, kwamba umaarufu hauwezi kufuta kifo, kwamba si pesa wala umaarufu vinaweza kurefusha maisha ya mtu kwa hata dakika moja, hata sekunde moja. Watu wanapohisi hivi zaidi, ndipo wanapotamani zaidi kuishi; watu wanapohisi hivi zaidi, ndipo wanapohofia kukaribia kwa kifo. Ni katika wakati huu tu ndipo wanapotambua kwa kweli kwamba maisha yao si yao, si yao kudhibiti, na kwamba mtu hana usemi kuhusu iwapo ataishi au atakufa, kwamba haya mambo yote yanapatikana nje ya udhibiti wa mtu.

4. Njoo Chini ya Utawala wa Muumba na Ukabiliane na Kifo kwa Utulivu

Wakati ule ambao mtu anazaliwa, nafsi ya mtu iliyo pweke inanza kupitia maisha hapa duniani, inapitia mamlaka ya Muumba ambayo Muumba ameipangilia. Ni wazi kwamba, kwa mtu husika, ile nafsi, hii ni fursa nzuri kabisa ya kupata maarifa kuhusu ukuu wa Muumba, kujua mamlaka Yake na kuyapitia binafsi. Watu wanaishi maisha yao kulingana na sheria za hatima zilizowekwa wazi kwao na Muumba, na kwa mtu yeyote mwenye akili razini aliye na dhamiri, kuelewa ukuu wa Muumba na kutambua mamlaka yake kwenye mkondo wa miongo yao

mbalimbali hapa nchini si jambo gumu kufanya. Kwa hivyo inafaa kuwa rahisi sana kwa kila mtu kutambua, kupitia kwa yale ambayo yeye mwenyewe amepitia maishani kwa kipindi cha miongo mbalimbali, kwamba hatima zote za binadamu zimeamuliwa kabla, na kung'amua au kujumlisha ni nini maana ya kuishi. Wakati uo huo ambao mtu anakumbatia mafunzo haya ya maisha, mtu ataelewa kwa utaratibu ni wapi maisha yanatokea, kunga'mua hasa ni nini ambacho moyo unahitaji kwa kweli, nini kitaongoza mtu kwenye njia ya kweli ya maisha, kazi maalum na shabaha ya maisha ya binadamu inafaa kuwa nini; na mtu ataanza kutambua kwa utaratibu kwamba kama mtu hataabudu Muumba, kama mtu hataingia kwenye utawala Wake, basi mtu anakabiliana na kifo—wakati nafsi iko karibu kukabiliana na Muumba kwa mara nyingine—moyo wa mtu utajazwa hofu na ugumu usio na mipaka. Kama mtu amekuwapo ulimwenguni kwa miongo kadhaa ilhali hajajua ni wapi maisha ya binadamu hutoka, angali hajatambua ni kwenye viganja vya mikono ya nani hatima ya binadamu huwa, basi si ajabu hataweza kukabiliana na kifo kwa utulivu. Mtu aliyepata maarifa ya ukuu wa Muumba baada ya kupitia miongo kadhaa ya maisha, ni mtu aliye na shukrani sahihi ya maana na thamani ya maisha; mtu aliye na kina cha maarifa kuhusu kusudi la maisha, aliye na hali halisi aliyopitia na anaelewa ukuu wa Muumba; na hata zaidi, mtu anayeweza kunyenyekea mbele ya mamlaka ya Muumba. Mtu kama huyo anaelewa maana ya uumbaji wa Mungu wa mwanadamu, anaelewa kwamba binadamu anafaa kumwabudu Muumba, kwamba kila kitu anachomiliki binadamu kinatoka kwa Muumba na kitarudi kwake siku fulani isiyo mbali sana kwenye siku za usoni; mtu kama huyo anaelewa kwamba Muumba hupangilia kuzaliwa kwa binadamu na ana ukuu juu ya kifo cha binadamu, na kwamba maisha na kifo vyote vimeamuliwa kabla na mamlaka ya Muumba. Kwa hiyo, wakati mtu anapong'amua mambo haya, mtu ataanza kuweza kukabiliana na kifo kwa utulivu na kwa kawaida, kuweka pembeni mali yake yote ya dunia kwa utulivu, kukubali na kunyenyekea kwa furaha kwa yote yatakayofuata, na kukaribisha awamu ya mwisho ya maisha iliyopangiliwa na Muumba badala ya kutishika vivyo hivyo tu na kung'ang'ana dhidi ya kifo. Ikiwa mtu anayaona maisha kama fursa ya kupitia ukuu wa Muumba na kujua mamlaka yake, ikiwa mtu anayaona maisha yake kama fursa nadra ya kutekeleza wajibu wake akiwa binadamu aliyeumbwa na kutimiza kazi yake maalum, basi mtu atakuwa ana mtazamo sahihi wa maisha, ataishi maisha yaliyobarikiwa na yanayoongozwa na Muumba, atatembea kwenye nuru ya Muumba, atajua ukuu wa Muumba, atakuwa katika utawala Wake, atakuwa shahidi wa matendo Yake ya kimiujiza na mamlaka Yake. Ni wazi kwamba, mtu kama huyo atahitajika kupendwa na kukubaliwa na Muumba, na mtu kama huyo ndiye anaweza kushikilia mtazamo mtulivu mbele ya kifo, na anayeweza kukaribisha awamu hii ya mwisho kwa furaha. Bila shaka Ayubu alikuwa na mtazamo kama huu kwa kifo; alikuwa katika nafasi ya kukubali kwa furaha awamu ya mwisho ya maisha, na baada ya kuhitimisha safari yake ya maisha vizuri, baada ya kukamilisha kazi yake maalum alirudi upande wa Muumba.

5. Bidii na Faida za Ayubu katika Maisha Zamruhusu Kukabiliana na Kifo kwa Utulivu

Katika Maandiko imeandikwa kuhusu Ayubu: “Kwa hivyo Ayubu akafariki, akiwa mzee na aliyejawa na siku” (Ayubu 42:17). Hii inamaanisha kwamba wakati Ayubu alipoaga dunia, hakuwa na majuto na hakuhisi maumivu, lakini aliondoka kimaumbile ulimwenguni. Kama vile kila mmoja anavyojua, Ayubu alikuwa mwanamume aliyemcha Mungu na aliyeambaa maovu alipokuwa hai; Mungu alimpongeza kwa matendo yake ya haki, watu waliyakumbuka, na maisha yake, zaidi ya yeyote yule mwingine, yalikuwa na thamani na umuhimu. Ayubu alifurahia baraka za Mungu na aliitwa mtakatifu na Yeye hapa duniani, na aliweza pia kujaribiwa na Mungu na kujaribiwa na Shetani; alisimama kuwa shahidi wa Mungu na alistahili kuwa mtu mtakatifu. Kwenye miongo mbalimbali baada ya kujaribiwa na Mungu, aliishi maisha ambayo yalikuwa yenye thamani zaidi, yenye maana zaidi, yaliyokita mizizi, na yenye amani zaidi kuliko hata awali. Kutokana na matendo yake ya haki, Mungu alimjaribu; kwa sababu ya matendo yake ya haki, Mungu alionekana kwake na kuongea naye moja kwa moja. Kwa hiyo, kwenye miaka yake baada ya kujaribiwa, Ayubu alielewa na kushukuru thamani ya maisha kwa njia thabiti zaidi, aliweza kutimiza ufahamu wa kina zaidi wa ukuu wa Muumba, na akapata maarifa yenye hakika na usahihi zaidi kuhusu namna ambavyo Muumba anavyotoa na kuzichukua baraka zake. Kitabu cha Ayubu kinarekodi kwamba Yehova Mungu alimpa hata baraka nyingi zaidi Ayubu kuliko hapo awali, Akimweka Ayubu katika nafasi bora zaidi ya kujua ukuu wa Muumba na kujua kukabiliana na kifo akiwa mtulivu. Kwa hiyo, Ayubu alipozeeka na kukabiliana na kifo, bila shaka asingekuwa na wasiwasi na mali yake. Hakuwa na wasiwasi wowote, hakuwa na chochote cha kujutia, na bila shaka hakuogopa kifo; kwani aliishi maisha yake akitembea ile njia ya kumcha Mungu, kuepuka maovu, na hakuwa na sababu yoyote ya kuwa na wasiwasi kuhusu mwisho wake mwenyewe. Ni watu wangapi leo wanaweza kuchukua hatua kwa njia zote hizo ambazo Ayubu alitumia alipokabiliwa na kifo chake mwenyewe? Kwa nini hakuna mtu anayeweza kuendeleza mwelekeo wa mtazamo rahisi kama huu? Kunayo sababu moja tu: Ayubu aliishi maisha kwenye harakati ya kutafuta kimsingi kusadiki, utambuzi, na unyenyekevu kwa ukuu wa Mungu, na ilikuwa katika kusadiki huku, utambuzi huu na unyenyekevu huu ambapo aliweza kupitia zile awamu muhimu za maisha, aliishi kwa kudhihirisha miaka yake ya mwisho na akajuliana hali na awamu yake ya mwisho ya maisha. Licha ya kile ambacho Ayubu alipitia, bidii zake na shabaha zake katika maisha zilikuwa za furaha na wala si zenye maumivu. Alikuwa na furaha si tu kwa sababu ya baraka au shukrani aliyopewa yeye na Muumba, lakini muhimu zaidi kwa sababu ya shughuli zake na shabaha za maisha, kwa sababu ya maarifa yaliyoongezeka kwa utaratibu na ufahamu wa kweli wa ukuu wa Muumba ambao alitimiza kupitia kwa kumcha Mungu na kwa kuepuka maovu, na zaidi, kwa sababu ya matendo Yake ya maajabu ambayo Ayubu alipitia kibinafsi wakati huu akiwa chini ya ukuu wa Muumba, na hali aliyopitia yenye

uchangamfu na isiyosahaulika na kumbukumbu za kuwepo kwake, kuzoeana na wenzake, na kuzoeana kati yake yeye na Mungu; kwa sababu ya tulizo na furaha zilizotokana na kujua mapenzi ya Muumba; kwa sababu ya kustahi kulikotokea baada ya kuona kwamba Yeye ni mkubwa, ni wa ajabu, Anayependeka, na ni mwaminifu. Sababu ya Ayubu kuweza kukabiliana na kifo bila ya kuteseka ni kwamba alijua kwamba, kwa kufa, angerudi kwenye upande wa Muumba. Na zilikuwa shughuli zake katika maisha zilizomruhusu kukabiliana na kifo akiwa ametulia, kukabiliana na matarajio ya Muumba kuchukua tena maisha yake, kwa moyo mzuri, na zaidi ya yote, kusimama wima, kutotikisika na kuwa huru kutokana na mashaka mbele ya Muumba. Je, watu wanaweza siku hizi kutimiza aina ya furaha ambayo Ayubu alikuwa nayo? Je, nyinyi wenyewe mko katika hali ya kufanya hivyo? Kwa sababu watu siku hizi wako hivyo, kwa nini hawawezi kuishi kwa furaha, kama alivyofanya Ayubu? Kwa nini hawawezi kutoroka mateso yanayotokana na woga wa kifo? Wakati wanapokabiliwa na kifo, baadhi ya watu hujiendea haja ndogo; wengine hutetemeka, wakazirai, na wakalalamika dhidi ya Mbinguni na binadamu vilevile, wengine hata wakalia kwa huzuni na kutokwa machozi. Kwa vyovyote vile, hii ndiyo miitikio ya ghafla inayofanyika wakati kifo kinapokaribia. Watu huwa na tabia hii ya kuaibisha haswa kwa sababu, ndani ya mioyo yao, wanaogopa kifo, kwa sababu hawana maarifa yaliyo wazi na uwezo wa kushukuru ukuu wa Mungu na mipangilio yake, na isitoshe hata kujinyenyekeza mbele ya vitu hivi; kwa sababu watu hawataki chochote ila kupangilia na kutawala kila kitu wenyewe, kudhibiti hatima zao binafsi, maisha yao binafsi na hata kifo. Si ajabu, hivyo basi, kwamba watu hawajawahi kuweza kuacha woga wa kifo.

6. Ni kwa Kukubali tu Ukuu wa Muumba Ndipo Mtu Anaweza Kurejea Upande Wake

Wakati mtu hana maarifa yaliyo wazi na hajapitia ukuu wa Mungu na mipangilio Yake, maarifa ya mtu kuhusu hatima na yale ya kifo yatakuwa yale yasiyoeleweka. Watu hawawezi kuona waziwazi kwamba haya yote yamo kwenye kiganja cha mkono wa Mungu, hawatambui kwamba Mungu ameushika usukani na Anashikilia ukuu juu yao, hawatambui kwamba binadamu hawezi kutupa nje au kutoroka ukuu kama huo; na kwa hivyo wakati wanapokabiliwa na kifo hakuna mwisho wowote katika maneno yao ya mwisho, wasiwasi wao, na hata majuto. Wanalemewa sana na mambo mengi, wanajivuta ajabu, kunakuwa na mkanganyo mkubwa, na haya yote yanawafanya kuogopa kifo. Kwani mtu yeyote aliyezaliwa ulimwenguni humu, kuzaliwa kwake kunahitajika, na kuaga kwake hakuwezi kuepukika, na hakuna mtu anayeweza kuupiga chenga mkondo huu. Kama mtu atataka kuondoka ulimwenguni humu bila maumivu, kama mtu atataka kukabiliana na awamu ya mwisho ya maisha bila kusitasita au wasiwasi, njia pekee ni kutokuwa na majuto. Na njia pekee ya kuondoka bila majuto ni kujua ukuu wa Muumba, kujua mamlaka yake, na kunyenyekeza mbele zake. Ni kwa njia hii tu ndipo mtu anaweza kuwa mbali na mahangaiko ya binadamu, maovu, utumwa wa Shetani; ni kwa njia hii

ndipo mtu anaweza kuishi maisha kama ya Ayubu, akiongozwa na akibarikiwa na Muumba, maisha yaliyo huru na yaliyokombolewa, maisha yenye thamani na maana, maisha yenye uaminifu na moyo wazi; ni kupitia kwa njia hii tu ndipo mtu anaweza kunyenyekea, kama Ayubu, kujaribiwa na kunyang'anywa na Muumba, kunyenyekeza katika mipango na mipangilio ya Muumba; ni kwa njia hii tu ndipo mtu anaweza kumwabudu Muumba maisha yake yote na kuweza kupata pongezi Lake, kama Ayubu alivyopata, na kusikia sauti Yake, kumwona akionekana; ni kwa njia hii tu ndipo mtu anaweza kuishi na kufa kwa furaha, kama Ayubu, bila ya maumivu, bila wasiwasi, bila majuto; ni kwa njia hii tu ndipo mtu anaweza kuishi kwa nuru, kama Ayubu, kupita kila mojawapo ya awamu ya maisha kwa nuru, na kukamilisha vizuri safari yake kwa nuru, kutimiza kwa ufanisi kazi yake maalum—kupitia, kujifunza, na kujua ukuu wa Muumba kama kiumbe kilichoumbwa—na kuiaga dunia kwa nuru, na milele hadi milele kusimama upande wa Muumba kama kiumbe kilichoumbwa, kilichopongezwa na Yeye.

Usikose Fursa ya Kujua Ukuu wa Muumba

Awamu sita zilizofafanuliwa hapo juu ni awamu muhimu zilizowekwa wazi na Muumba ambazo kila mtu wa kawaida lazima apitie katika maisha yake. Kila mojawapo ya awamu hizi ni za kweli; hakuna mojawapo kati yazo ambayo inaweza kuepukwa, na zote zinasheheni uhusiano na kuamuliwa kabla kwa Muumba na ukuu Wake. Hivyo basi kwa binadamu, kila mojawapo ya awamu hizi ni sehemu muhimu ya kujikagua, na namna ya kupitia kila mojawapo vizuri ni suala muhimu sana ambalo nyinyi nyote mnakabiliwa nalo.

Mkusanyiko wa miongo ambayo inaunda maisha ya binadamu si mirefu sana wala mifupi sana. Miaka ishirini na kitu iliyopo katikati ya kuzaliwa na kukomaa hupita kwa muda mfupi tu wa kupepesa jicho, na ingawaje wakati huu katika maisha mtu anachukuliwa kuwa mtu mzima, watu katika kundi hili la umri wanajua machache sana kuhusu maisha ya binadamu na hatima ya binadamu. Wanapozidi kupata uzoefu zaidi, ndipo wanapopiga hatua kwa utaratibu hadi kwenye umri wa miaka ya kati. Watu katika miaka yao ya thelathini na arubaini huanza kuupata uzoefu unaoanza kuota wa maisha na hatima yake, lakini fikira zao kuhusu mambo haya zingali na ukungu mwingi sana akilini mwao. Si mpaka umri wa arubaini ndipo baadhi ya watu huanza kumwelewa binadamu na ulimwengu, vilivyoumbwa na Mungu, na kung'amua kwamba maisha ya binadamu yanahusu tu, kile ambacho hatima ya binadamu inahusu. Baadhi ya watu, ingawaje wamekuwa wafuasi wa muda mrefu wa Mungu na sasa wanao umri wa kati, bado hawamiliki maarifa na ufafanuzi sahihi wa ukuu wa Mungu, sikwambii hata unyenyekevu wa kweli. Baadhi ya watu hawajali chochote isipokuwa namna ya kupokea baraka, na ingawaje wameishi kwa miaka mingi, hawajui au hawaelewi hata kidogo hoja ya ukuu wa Muumba juu ya hatima ya binadamu, na kwa hivyo bado hawajaingia hata kwenye kipindi cha matendo halisi cha

kunyenyekea katika mipango na mipangilio ya Mungu. Watu kama hao ni wajinga kabisa; watu kama hao wanaishi maisha yao bure bilashi.

Kama maisha ya binadamu yangegawanywa kulingana na kiwango cha mtu cha kile alichopitia maishani na maarifa yake kuhusu hatima ya binadamu, basi yangegawanywa kwa sura tatu. Sura ya kwanza ni ujana, miaka ile ya kati ya kuzaliwa na umri wa kati, au kuanzia kuzaliwa hadi kugonga miaka thelathini. Sura ya pili ni ya ukomavu, kuanzia umri wa miaka ya kati hadi umri wa uzee, au kuanzia thelathini hadi sitini. Na sura ya tatu ni kile kipindi cha uzee wa mtu, kuanzia umri wa uzee, kuanzia miaka sitini hivi, mpaka pale mtu anapoondoka ulimwenguni. Kwa maneno mengine, kuanzia kuzaliwa hadi umri wa miaka ya kati, maarifa ya watu wengi kuhusu hatima na maisha ni finyu na ni yale ya kuiga tu kama kasuku, fikira za wengine yanayokosa hali halisi iliyo ya kweli na ya matendo. Kwenye kipindi hiki, mtazamo wa mtu kuhusu maisha, na namna ambavyo mtu anapojipanga katika ulimwengu vyote ni vya juujuu na vinyonge sana. Hiki ndicho kipindi cha mtu cha utoto. Baada tu ya mtu kuonja furaha na huzuni zote za maisha ndipo anapofaidi na kupata ufahamu halisi wa hatima, ndipo mtu—kwa kufichika akilini, na ndani kabisa ya moyo wake—huanza kwa utaratibu kushukuru kutoweza kurudishwa nyuma kwa hatima, na kuanza kutambua polepole kwamba ukuu wa Muumba juu ya hatima ya binadamu kwa kweli upo. Kwa kweli hiki ndicho kipindi cha kuanza kukomaa kwa mtu. Baada ya mtu kusita kupambana dhidi ya hatima, na pale ambapo mtu hayuko radhi tena kuvutwa kwenye mabishano, lakini anajua msimamo wake, anajinyenyekeza kwa mapenzi ya Mbinguni, na kujumlisha mafanikio na makosa ya maisha ya mtu huyo, na anasubiria hukumu ya Muumba kwa maisha ya mtu—hiki ni kipindi cha ukomavu. Tukitilia maanani aina hizi tofauti za kile mtu amepitia na kufaidi ambako watu hupata kwenye vipindi hivi vitatu, katika hali za kawaida fursa ya mtu ya kujua ukuu wa Muumba si kubwa sana. Kama mtu ataishi kufikisha umri wa miaka sitini, mtu anayo miaka thelathini tu au karibu na hapo kuujua ukuu wa Mungu; kama mtu atataka kipindi kirefu zaidi cha muda, hilo linawezekana tu kama maisha ya mtu yatakuwa marefu zaidi, tuseme kama mtu ataweza kuishi karne moja. Kwa hivyo Ninasema, kulingana na kanuni za sheria za kawaida za uwepo wa binadamu, ingawaje ni mchakato mrefu sana kuanzia wakati ule mtu anakumbana na mada ya kujua ukuu wa Muumba hadi pale ambapo mtu anaweza kutambua hoja ya ukuu wa Muumba, na kutoka hapo mpaka pale ambapo mtu anaweza kujinyenyekeza kwa utawala huo, kama kwa hakika mtu atahesabu miaka hiyo, miaka hiyo haizidi thelathini au arubaini hivi ambapo mtu anayo fursa ya kufaidi haya yote. Na mara nyingi, watu hujisahau kutokana na matamano yao na malengo yao ya kupokea baraka; hawawezi kutambua ni wapi ambapo kiini halisi cha maisha ya binadamu kipo, hawang'amui umuhimu wa kujua ukuu wa Muumba, na kwa hivyo hawafurahii fursa hii yenye thamani ya kuingia kwenye ulimwengu wa binadamu kuhusiana na maisha ya binadamu na kile alichopitia,

kupitia ukuu wa Muumba, na hawatambui namna lilivyo jambo la thamani kwa kiumbe chochote kilichoumbwa kupokea mwongozo wa kibinafsi kutoka kwa Muumba. Kwa hivyo Ninasema, watu wale wanaotaka kazi ya Mungu kuisha haraka, wanaopenda Mungu angepangilia mwisho wa binadamu haraka iwezekanavyo, ili waweze mara moja kutazama hali Yake halisi na muda si muda kubarikiwa, wanayo hatia ya aina mbaya zaidi ya kutotii na ujinga wa kupindukia. Na kwa wale wanaotamani, kwenye muda wao finyu, kung'amua fursa hii ya kipekee ili kuujua ukuu wa Muumba, hao ni watu werevu, wenye akili zao. Matamania haya mawili tofauti yanafichua mitazamo miwili tofauti na shughuli za kufuatilia: Wale wanaotafuta baraka ni wachoyo na waovu; hawatilii maanani mapenzi yoyote ya Mungu, wala hawatafuti kujua ukuu wa Mungu, wasiwahi kutamani kujinyenyekeza katika utawala huo, wanataka kuishi tu wanavyopenda. Wao ni watovu wa wema; wao ndio wanaofaa kuangamizwa. Wale wanaotafuta kumjua Mungu wanaweza kuweka pembeni matamania yao, wako radhi kujinyenyekeza kwa ukuu wa Mungu na mipangilio ya Mungu; wanajaribu kuwa aina ya watu ambao wananyenyekeza katika mamlaka ya Mungu na kutimiza tamania la Mungu. Watu kama hao huishi kwa nuru, huishi katikati ya baraka za Mungu; kwa hakika wataweza kupongezwa na Mungu. Haijalishi ni nini, chaguo la binadamu halina manufaa, binadamu hawana kauli yoyote kuhusiana na muda gani ambao kazi ya Mungu itachukua. Ni bora zaidi kwa watu kujiweka katika udhibiti wa Mungu, kunyenyekeza katika ukuu Wake. Usipojiweka katika huruma Yake, ni nini utakachofanya? Je, Mungu atakuwa na hasara yoyote? Usipojiweka katika huruma Yake, ukijaribu kuushika usukani, unafanya chaguo la kijinga, na wewe tu ndiwe utakayepata hasara hatimaye. Endapo tu watu watashirikiana na Mungu haraka iwezekanavyo, endapo tu watafanya hima kukubali mipango Yake, kujua mamlaka Yake, na kutambua yote ambayo Amewafanyia, ndipo watakuwa na tumaini, ndipo maisha yao yatapata maana na kuepuka kuwa hapo tu, ndipo watakapopata wokovu.

Hakuna Anayeweza Kubadilisha Hoja Kwamba Mungu Anashikilia Ukuu juu ya Hatima ya Binadamu

Baada ya kusikiliza kila kitu Nilichomaliza kusema, je, fikira yenu ya hatima imebadilika? Mnaelewa vipi hoja ya ukuu wa Mungu juu ya hatima ya binadamu? Ili kuiweka kwa urahisi, katika mamlaka ya Mungu kila mtu anakubali waziwazi au kimyakimya ukuu Wake na mipangilio Yake, na haijalishi ni vipi ambavyo mtu anashughulika katika mkondo wa maisha yake, haijalishi ni njia ngapi mbovu ambazo mtu ametembelea, mwishowe atarudi tu kwenye mzingo wa hatima ambayo Muumba amempangia yeye. Hii ndiyo hali isiyoshindika ya mamlaka ya Muumba, namna ambavyo mamlaka Yake yanavyodhibiti na kutawala ulimwengu. Ni hii hali ya kutoshindika, mfumo huu wa kudhibiti na kutawala, ambao unawajibikia sheria zinazoamuru maisha ya mambo yote, zinazoruhusu binadamu kuweza kuhama hadi kwenye mwili tofauti

baada ya kifo tena na tena bila uingiliaji kati, zinazofanya ulimwengu kugeuka mara kwa mara na kusonga mbele, siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka. Mmeshuhudia hoja hizi zote na unazielewa, haijalishi kama ni za juujuu ama ni za kina; kina cha ufahamu wako kinategemea kile unachopitia na maarifa ya ukweli, na maarifa yako kuhusu Mungu. Kujua kwako vyema uhalisia wa ukweli, ni kiwango kipi ambacho umepitia matamshi ya Mungu, ni vipi unajua vyema hali halisi ya Mungu na tabia yake—hii inawakilisha kina cha ufahamu wako wa ukuu na mipangilio ya Mungu. Je, uwepo wa ukuu wa Mungu na mipangilio unategemea kama binadamu wanaiyenyekea? Je, hoja kwamba Mungu anamiliki mamlaka haya inaamuliwa na kama binadamu watayanyenyekea? Mamlaka ya Mungu yapo licha ya hali mbalimbali; katika hali zote, Mungu anaamuru na kupangilia hatima ya kila binadamu na mambo yote kulingana na fikira Zake, mapenzi Yake. Hali hii haitabadilika kwa sababu binadamu hubadilika, na iko huru wala haitegemei mapenzi ya binadamu, haiwezi kubadilishwa na mabadiliko yoyote ya muda, anga, na jiografia, kwani mamlaka ya Mungu ndiyo hali yake halisi kabisa. Kama binadamu anaweza kujua na kuukubali ukuu wa Mungu, na kama binadamu anaweza kuunyenyekea, haiwezi kwa vyovyote vile kubadilisha hoja kwamba ukuu wa Mungu upo juu ya hatima ya binadamu. Hivi ni kusema kwamba, haijalishi ni mtazamo gani ambao binadamu atachukua kwa ukuu wa Mungu, hauwezi tu kubadilisha hoja kwamba Mungu anashikilia ukuu juu ya hatima ya binadamu na juu ya mambo yote. Hata kama hutanyenyekea katika ukuu wa Mungu, angali Anaamuru hatima yako; hata kama huwezi kujua ukuu Wake, mamlaka Yake yangali yapo. Mamlaka ya Mungu na hoja ya ukuu wa Mungu dhidi ya hatima ya binadamu viko huru dhidi ya mapenzi ya binadamu, havibadiliki kulingana na mapendeleo na machaguo yako ya binadamu. Mamlaka ya Mungu yapo kila mahali, kila saa, kila muda. Kama mbingu na nchi zingepita, mamlaka Yake yasingewahi kupita, kwani Yeye ni Mungu Mwenyewe, Anamiliki mamlaka ya kipekee, na mamlaka Yake hayazuiliwi au kuwekewa mipaka na watu, matukio, au vitu, na anga au na jiografia. Siku zote Mungu hushikilia mamlaka Yake, huonyesha uwezo Wake, huendeleza usimamizi Wake wa kazi kama kawaida; kila wakati Anatawala viumbe wote, hutosheleza viumbe wote, huunda na kupangilia viumbe wote, kama Alivyofanya siku zote. Hakuna anayeweza kubadilisha hili. Hii ni hoja; huu umekuwa ukweli usiobadilika tangu zama za kale!

Mtazamo na Matendo Bora ya Mtu Anayependa Kujinyenyekeza katika Mamlaka ya Mungu

Mwanadamu anatakiwa kuwa na mtazamo gani sasa katika kujua na kujali mamlaka ya Mungu, hoja ya ukuu wa Mungu juu ya hatima ya binadamu? Hili ni tatizo la kweli linalokabili kila mmoja. Wakati wa kukabiliana na matatizo ya kweli ya maisha, unafaa kujua na kuelewa vipi mamlaka ya Mungu na ukuu Wake? Wakati hujui namna ya kuelewa, kushughulikia, na kupitia matatizo haya, ni mtazamo gani unaofaa kutumia ili kuonyesha nia yako, tamanio lako,

na uhalisia wako wa kujinyenyekeza katika ukuu na mipangilio ya Mungu? Kwanza lazima ujifunze kusubiri; kisha lazima ujifunze kutafuta; kisha lazima ujifunze kujinyenyekeza. “Kusubiri” kunamaanisha kusubiria muda wa Mungu, kusubiria watu, matukio, na mambo ambayo Amekupangilia wewe, kusubiria mapenzi Yake ili yaweze kwa utaratibu kujifichua kwako. “Kutafuta” kunamaanisha kuangalia na kuelewa nia za Mungu katika fikira Zake kwako wewe kupitia watu, matukio, na mambo ambayo Amekuwekea wazi, kuelewa ukweli kupitia mambo hayo, kuelewa kile ambacho binadamu lazima watimize na njia ambazo lazima wafuate, kuelewa matokeo ambayo Mungu ananua kufanikisha katika binadamu na mafanikio Anayonua kufikia ndani yao. “Kujinyenyekeza,” bila shaka, kunaashiria kukubali watu, matukio, na mambo ambayo Mungu amepanga, kukubali ukuu Wake na, kwa yote, kupata kujua namna ambavyo Muumba anaamuru hatima ya binadamu, namna Anavyomjaliza binadamu na maisha Yake, na namna Anavyofanya kazi ya ukweli katika binadamu. Mambo yote katika mipangilio na ukuu wa Mungu hutii sheria za kimaumbile, na kama utaamua kumwachia Mungu kupangilia na kuamuru kila kitu kwa niaba yako, unafaa kujifunza kusubiri, unafaa kujifunza kutafuta, unafaa kujifunza kujinyenyekeza. Huu ndio mtazamo ambao kila mtu anayetaka kujinyenyekeza katika mamlaka ya Mungu lazima awe nao, ubora wa kimsingi ambao kila mmoja anayetaka kuukubali ukuu na mipangilio ya Mungu lazima aumiliki. Ili kushikilia mtazamo kama huu, kumiliki ubora kama huu, lazima mfanye kazi kwa bidii zaidi; na ndipo mnapoweza kuingia kwenye uhalisi wa kweli.

Kumkubali Mungu kama Bwana Wenu wa Kipekee Ndiyo Hatua ya Kwanza katika Kutimiza Wokovu

Ukweli kuhusiana na mamlaka ya Mungu ni ukweli ambao kila mmoja lazima atilie maanani kwa umakinifu, lazima apitie na aelewe katika moyo wake; kwani ukweli huu unao mwelekeo katika maisha ya kila mmoja, kwenye maisha ya kale, ya sasa, na ya siku za usoni ya kila mmoja, kwenye awamu muhimu ambazo kila mtu lazima apitie maishani, katika maarifa ya binadamu kuhusu ukuu wa Mungu na mtazamo ambao anafaa kuwa nao katika mamlaka ya Mungu, na kawaida, kwa kila hatima ya mwisho ya kila mmoja. Kwa hivyo inachukua nguvu za maisha yako yote kujua na kuyaelewa. Unapochukua mamlaka ya Mungu kwa umakinifu, unapoukubali ukuu wa Mungu, kwa utaratibu utanza kutambua na kuelewa kwamba mamlaka ya Mungu kwa kweli yapo. Lakini kama hutawahi kutambua mamlaka ya Mungu, hutawahi kukubali ukuu Wake, basi haijalishi ni miaka mingapi utakayoishi, hutafaidi hata chembe maarifa ya ukuu wa Mungu. Kama hutajua na kuelewa kwa kweli mamlaka ya Mungu, basi utakapofika mwisho wa barabara, hata kama utakuwa umesadiki katika Mungu kwa miongo mingi, hutakuwa na chochote cha kuonyesha katika maisha yako, maarifa yako ya ukuu wa Mungu juu ya hatima ya binadamu yatakuwa kwa hakika sufuri bin sufuri. Huoni kuwa jambo hili ni la huzuni mno? Kwa hivyo haijalishi umetembea kwa umbali gani maishani, haijalishi

unao umri wa miaka mingapi sasa, haijalishi safari inayosalia itakuwa ya umbali gani, kwanza lazima utambue mamlaka ya Mungu na kuyamakinikia, ukubali hoja kwamba Mungu ni Bwana wako wa kipekee. Kutimiza maarifa yaliyo wazi, sahihi na kuelewa ukweli huu kuhusiana na ukuu wa Mungu juu ya hatima ya binadamu ni funzo la lazima kwa kila mmoja, ndio msingi wa kuyajua maisha ya binadamu na kutimiza ukweli, ndiyo maisha ya kila siku na mafunzo ya kimsingi ya kumjua Mungu ambayo kila mmoja anakabili nayo, na ambayo hakuna yeyote anayeweza kuyakwepa. Kama mmoja wenu angependa kuchukua njia za mkato ili kufikia shabaha hii, basi Ninakuambia, hilo haliwezekani! Kama mmoja wenu anataka kukwepa ukuu wa Mungu, basi hilo nalo ndilo haliwezekani zaidi! Mungu ndiye Bwana wa pekee wa binadamu, Mungu ndiye Bwana wa pekee wa hatima ya binadamu, na kwa hivyo haiwezekani kwa binadamu kuamuru hatima yake mwenyewe, haiwezekani kwake kuishinda. Haijalishi uwezo wa mtu ni mkubwa kiasi kipi, mtu hawezi kuathiri, sikwambii kuunda, kupangilia, kudhibiti, au kubadilisha hatima za wengine. Yule Mungu Mwenyewe wa kipekee ndiye Anayeweza kuamuru tu mambo yote kwa binadamu, kwani Yeye tu ndiye anayemiliki mamlaka ya kipekee yanayoshikilia ukuu juu ya hatima ya binadamu; na kwa hivyo Muumba pekee ndiye Bwana wa kipekee wa binadamu. Mamlaka ya Mungu yanashikilia ukuu sio tu juu ya binadamu walioumbwa, lakini juu ya hata viumbe ambavyo havikuumbwa visivyoweza kuonekana na binadamu, juu ya nyota, juu ya ulimwengu mzima. Hii ni hoja isiyopingika, hoja ambayo kweli ipo, ambayo hakuna binadamu au kiumbe chochote kinaweza kubadilisha. Kama mmoja wenu angali hajatosheka na mambo kama yalivyo, akiamini kwamba una ujuzi fulani maalum au uwezo, na bado anafikiria unaweza kubahatika na kubadilisha hali zako za sasa au vinginevyo kuzitoroka; kama utajaribu kubadilisha hatima yako kupitia kwa jitihada za binadamu, na hivyo basi kujitokeza kati ya wengine na kupata umaarufu na utajiri; basi Ninakwambia, unayafanya mambo kuwa magumu kwako, unajitakia taabu tu, unajichimbia kaburi lako mwenyewe! Siku moja, hivi karibuni au baadaye, utagundua kwamba ulifanya chaguo baya, kwamba jitihada zako ziliambulia patupu. Malengo yako, tamani lako la kupambana dhidi ya hatima, na mwenendo wako binafsi wa kupita kiasi, utakuongoza kwenye barabara isiyoweza kukurudisha kule ulikotoka, na kwa hili utaweza kujutia baadaye. Ingawaje sasa huoni ubaya wa athari hiyo, unapopitia na kushukuru zaidi na zaidi ukweli kwamba Mungu ndiye Bwana wa hatima ya maisha, utaanza kwa utaratibu kutambua kile Ninachozungumzia leo na athari zake za kweli. Haijalishi kama kwa kweli unao moyo na, haijalishi kama wewe ni mtu anayependa ukweli, inategemea tu ni mtazamo aina gani ambao utachukua kuhusiana na ukuu wa Mungu na ule ukweli. Na kwa kawaida, hili linaamua kama kweli unaweza kujua na kuelewa mamlaka ya Mungu. Kama hujawahi katika maisha yako kuhisi ukuu wa Mungu na mipangilio yake, na isitoshe hujawahi kutambua na kukubali mamlaka ya Mungu, basi utakosa thamani kabisa, bila shaka utakuwa athari ya chukizo na zao la kukataliwa na Mungu, hayo yote ni kutokana na njia

uliyochukua na chaguo ulilofanya. Lakini wale ambao, katika kazi ya Mungu, wanaweza kukubali jaribio Lake, kukubali ukuu Wake, kujinyenyekeza katika mamlaka Yake, na kufaidi kwa utaratibu hali halisi waliyopitia na matamshi Yake, watakuwa wametimiza maarifa halisi ya mamlaka ya Mungu, ufahamu halisi wa ukuu Wake, na watakuwa kwa kweli watakuwa wanatii Muumba. Watu kama hao tu ndio watakaokuwa wameokolewa kwa kweli. Kwa sababu wameujua ukuu wa Mungu, kwa sababu wameukubali, shukrani yao ya na kujinyenyekeza kwao katika hoja ya Mungu juu ya hatima ya binadamu ni ya halisi na sahihi. Wanapokabiliana na kifo wataweza, kama Ayubu, kuwa na akili isiyotishika na kifo, kujinyenyekeza katika mipango na mipangilio ya Mungu katika mambo yote, bila chaguo lolote la kibinafsi, bila tamanio lolote la kibinafsi. Mtu kama huyo tu ndiye atakayeweza kurudi katika upande wa Muumba kama kiumbe cha kweli cha binadamu kilichoumbwa.

Desemba 17, 2013

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee IV

Utakatifu wa Mungu (I)

Tumekuwa na ushirika wa ziada wa mamlaka ya Mungu wakati wa mkutano wetu wa mwisho, na hatutazungumza kuhusu haki ya Mungu sasa hivi. Leo tutazungumza kuhusu mada nzima mpya—utakatifu wa Mungu. Utakatifu wa Mungu pia ni kipengele kingine cha kiini cha kipekee cha Mungu, hivyo kuna umuhimu mkubwa wa kushiriki mada hii hapa. Hiki kipengele cha kiini cha Mungu ambacho Nitashiriki, pamoja na vile vipengele viwili tulivyoshiriki mbeleni cha tabia ya haki ya Mungu na mamlaka ya Mungu—yote ni ya kipekee? (Ndiyo.) Utakatifu wa Mungu pia ni wa kipekee, kwa hivyomaudhui ya ushirika wetu wa leo ndiyo yatakayojumuisha msingi na kiini cha upekee huu. Leo tunaenda kushiriki kuhusu kiini cha kipekee cha Mungu—utakatifu Wake. Labda baadhi yenu wana wasiwasi kidogo, na wanauliza, “Mbona kushiriki utakatifu wa Mungu?” Msijali, Nitawazungumzia kuuhusu polepole. Punde tu mtakapousikia mtajua mbona ni muhimu Kwangu kushiriki mada hii.

Kwanza wacha tufafanue neno “takatifu.” Mkitumia utambuzi wenu na kutoka kwa maarifa yenu mmefunzwa, mnaelewa ufafanuzi wa “takatifu” kuwa nini? (“Takatifu” inamaanisha bila doa, bila upotovu au dosari yoyote ya binadamu. Kila kitu inachonururisha—kiwe kwa mawazo, matamshi ama vitendo, kila kitu inafanya—ni chema kabisa.) Vizuri kabisa. (“Takatifu” ni ya Mungu, haijanajisiwa, isiyokosewa na mtu. Ni ya kipekee, ni ishara ya tabia ya Mungu.) Huu ni ufafanuzi wako. Katika moyo wa kila mtu, neno hili “takatifu” lina wigo, ufafanuzi na fasiri. Kwa kiwango cha chini kabisa, mnapoona neno “takatifu” akili zenu si tupu. Mna wigo fulani uliofafanuliwa wa neno hili, na misemo ya watu wengine inakaribiana kiasi na misemo

inayofafanua kiini cha tabia ya Mungu. Hii ni vizuri sana. Watu wengi zaidi wanaamini neno “takatifu” ni neno njema, na hii inaweza kuthibitishwa. Lakini utakatifu wa Mungu Ninaotaka kushiriki leo hautafafanuliwa tu, ama kuelezwa tu. Badala yake, Nitatumia baadhi ya ukweli kudhihirisha ili kukuruhusu kuona kwa nini Nasema Mungu ni mtakatifu, na mbona Natumia neno “takatifu” kuelezea kiini cha Mungu. Kabla ya ushirika wetu kuisha, utahisi kwamba matumizi ya neno “takatifu” kuelezea kiini cha Mungu na matumizi ya neno hili kumrejelea Mungu yanastahili sana na yanafaa. Kwa kiwango cha chini zaidi, kuhusiana na lugha za sasa za binadamu, kutumia neno hili kumrejelea Mungu kunafaa hasa—ni neno pekee kwa lugha ya binadamu linalofaa kabisa kumrejelea Mungu. Si neno tupu linapotumika kumrejelea Mungu, wala si sifa bila sababu au pongezi tupu. Madhumuni ya ushirika wetu ni kumruhusu kila mtu kuutambua ukweli wa kipengele hiki cha kiini cha Mungu. Mungu haogopi uelewa wa watu, bali kutoelewa kwao tu. Mungu anataka kila mtu ajue kiini Chake na kile Anacho na alichio. Hivyo kila wakati tunapotaja kipengele cha kiini Cha Mungu, tunaweza kutumia ukweli mwingi kuwaruhusu watu kuona kwamba kipengele hiki cha kiini cha Mungu kweli kipo.

Kwa sababu sasa tuna ufafanuzi wa neno “takatifu,” wacha tuangalie baadhi ya mifano. Katika fikira za watu, wanafikiria vitu na watu wengi kuwa “takatifu”. Kwa mfano, wavulana na wasichana mabikira wanaelezwa kama watakatifu katika kamusi za binadamu. Lakini je, kweli ni watakatifu? Je, hivi vinavyoitwa takatifu na “vitakatifu” tutakayoshiriki kuhusu leo ni kitu kimoja? (La.) Wale miongoni mwa wanadamu walio na maadili ya juu, wale walio na matamshi bora na ya maarifa, wasiomwumiza yeyote, na ambao, kupitia kwa maneni wanayozungumza, wanawafanya wengine kustareheka na kufurahia—ni watakatifu? Wale wanaofanya mazuri mara nyingi, wanaopenda kutoa na kuwasaidia wengine, wale wanaoleta raha tele ndani ya maisha ya watu—ni watakatifu? Wale wasio na fikira za kujihudumia, wasioweka madai makali juu ya yeyote, wanaomvumilia yeyote—ni watakatifu? Wale ambao hawajawahi kuwa na mzozo na yeyote wala kujinufaisha na yeyote—ni watakatifu? Basi wale wanaofanya kazi kwa minajili ya uzuri wa wengine, wanaofaidi wengine na kuleta uboreshaji kwa wengine kwa namna zote—ni watakatifu? Wanaowapa wengine akiba zao zote za maisha na kuishi maisha rahisi, walio wakali kwa wao wenyewe lakini wanawashughulikia wengine kwa ukarimu—ni watakatifu? (La.) Mnakumbuka kwamba mama zenu waliwatunza na kuwalinda kwa njia zote zinazoweza kufikiriwa—ni watakatifu? Vijimungu mnaopenda sana, wawe watu maarufu, mashuhuri ama watu wakubwa—ni watakatifu? (La.) Hebu sasa tuangalie wale manabii katika Biblia walioweza kuelezea siku za baadaye ambazo hazikujulikana na wengine wengi—mtu wa aina hii alikuwa mtakatifu? Watu walioweza kurekodi maneno ya Mungu na ukweli wa kazi Yake katika Biblia—walikuwa watakatifu? Musa alikuwa mtakatifu? Ibrahimu alikuwa mtakatifu? (La.) Ayubu je? Alikuwa mtakatifu? (La.) Ayubu aliitwa mtu mwenye haki na Mungu, basi mbona

hata yeye anasemekana kutokuwa mtakatifu? Watu wanaomcha Mungu na kuepukana na maovu kweli si watakatifu? Ni watakatifu ama si watakatifu? (La.) Mna wasiwasi kidogo, hamna uhakika sana, na hamthubutu kusema “La,” lakini pia hamthubutu kusema “Ndiyo,” kwa hivyo mwishowe mnasema “La” shingo upande. Acha Niulize swali lingine. Wajumbe wa Mungu—wajumbe ambao Mungu huwatumia chini duniani—ni watakatifu? Malaika ni watakatifu? (La.) Binadamu wasio na upotoshaji wa Shetani—ni watakatifu? (La.) Nyinyi mnajibu “La” kila mara kwa kila swali. Kwa msingi upi? Mmechanganyikiwa, sivyo? Basi mbona hata malaika wanasemekana sio watakatifu? Mna wasiwasi hapa, sio? Basi mnaweza kugundua ni kwa msingi upi watu, vitu ama viumbe wasioubwa tuliotaja mbeleni si watakatifu? Nina uhakika hamwezi. Hivyo, si kusema kwenu “La” basi ni kukosekana kwa uwajibikaji kidogo? Hamjibu bila kujali? Watu wengine wanafikiria: “Unauliza kwa namna hii, kwa hivyo si lazima iwe hivyo hakika.” Msijibu tu bila kujali. Fikirieni kwa makini iwapo jibu ni ndiyo au la. Mtajua tutakaposhiriki mada ifuatayo mbona ni “La.” Nitawapa jibu hivi punde. Hebu kwanza tusome baadhi ya maandiko.

Amri ya Yehova Mungu kwa Mwanadamu

Mwa 2:15-17 Naye Yehova Mungu akamchukua mtu huyo, na kumweka ndani ya bustani ya Eden ili ailime na kuihifadhi. Yehova Mungu akamwamrisha mtu huyo, akisema, Unaweza kula kwa uhuru matunda kutoka miti yote ya bustani: Lakini kutoka mti wa maarifa ya mema na maovu, usiyale: kwa kuwa katika siku ambapo utakula matunda kutoka mti huo bila shaka utakufa.

Nyoka Anamshawishi Mwanamke

Mwa 3:1-5 Sasa nyoka alikuwa mwenye hila kuliko wanyama wote wa mwitu ambao Yehova Mungu alikuwa amewaumba. Naye akamwambia mwanamke, Naam, Mungu amesema, Msile matunda ya miti yote ya bustani? Naye mwanamke akamwambia nyoka, Tunaweza kula matunda ya miti katika bustani: Mungu amesema, Lakini msile wala kuyagusa matunda ya mti ulio katikati ya bustani, msije mkafa. Naye nyoka akamwambia mwanamke, Bila shaka hamtakufa: Kwa kuwa Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, macho yenu yatafunuliwa, nanyi mtakuwa kama miungu, mkijua mema na maovu.

Hivi vifungu viwili ni dondoo kutoka kwa kitabu cha Mwanzo katika Biblia. Je, nyinyi nyote mnavijua vifungu hivi viwili? Hiki ni kitu kilichofanyika mwanzoni wakati binadamu kwanza aliumbwa; lilikuwa ni tukio halisi. Kwanza hebu tuangalie ni amri ya aina gani ambayo Yehova Mungu aliwapa Adamu na Hawa, kwani yaliyomo katika amri hii ni muhimu sana kwa mada yetu ya leo. “Yehova Mungu akamwamrisha mtu huyo, akisema, Unaweza kula kwa uhuru

matunda kutoka miti yote ya bustani: Lakini kutoka mti wa maarifa ya mema na maovu, usiyale: kwa kuwa katika siku ambapo utakula matunda kutoka mti huo bila shaka utakufa.” Amri ya Mungu kwa mwanadamu katika kifungu hiki ina nini? Kwanza, Mungu anamwambia mwanadamu kile anachoweza kula, yakiwa ni matunda ya miti ya aina nyingi. Hakuna hatari na hakuna sumu, yote yanaweza kulika na kulika atakavyo mtu, bila wasiwasi wowote. Hii ni sehemu moja. Sehemu nyingine ni onyo. Onyo hili linamwambia mwanadamu mti ambao hawezi kula tunda kutoka—lazima asile tunda kutoka kwa mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Nini itafanyika akifanya hivyo? Mungu alimwambia mwanadamu: Ukilila hakika utakufa. Maneno haya yanaeleweka kwa urahisi? Iwapo Mungu angekwambia jambo hili lakini hukuelewa kwa nini, ungelichukulia kama kanuni ama amri ya kufuatwa? Linapaswa kufuatwa, sivyo? Lakini iwapo mwanadamu anaweza ama hawezi kulifuata, maneno ya Mungu hayaachi shaka. Mungu alimwambia mwanadamu kwa uwazi kabisa kile anachoweza kula na kile asichoweza, na kile kitakachofanyika akila kile hapaswi kula. Umeona tabia yoyote ya Mungu katika haya maneno machache ambayo Alisema? Haya maneno ya Mungu ni ya ukweli? Kuna udanganyifu wowote? Kuna uongo wowote? Kuna chochote kinachotisha? (La.) Mungu kwa uaminifu, kwa kweli, kwa dhati Alimwambia mwanadamu kile anachoweza kula na kile asichoweza kula, wazi na dhahiri. Kuna maana iliyofichwa katika maneno haya? Maneno haya yanaeleweka kwa urahisi? Je, kuna haja yoyote ya dhana? (La.) Hakuna haja ya kukisia. Maana yake ni wazi kwa mtazamo mmoja, na unaelewa punde tu unapoyaona. Ni wazi kabisa. Yaani, kile Mungu anataka kusema na Anachotaka kuonyesha kinatoka katika moyo Wake. Mambo ambayo Mungu anaonyesha ni safi, yanaeleweka kwa urahisi na ni wazi. Hakuna nia za siri ama maana zilizofichwa. Alizungumza moja kwa moja na mwanadamu, Akimwambia kile anachoweza kula na kile asichoweza kula. Hivyo ni kusema, kupitia maneno haya ya Mungu mwanadamu anaweza kuona kwamba moyo wa Mungu ni angavu, kwamba moyo wa Mungu ni wa kweli. Hakuna uwongo kabisa hapa; si kukwambia kwamba huwezi kula kile kinacholika ama kukwambia “Ifanye na uone kitakachofanyika” na vitu ambavyo huwezi kula. Hamaanishi hivi. Chochote afikiriacho Mungu katika moyo Wake ndicho Anachosema. Nikisema Mungu ni mtakatifu kwa sababu Anaonyesha na kujifichua Mwenyewe ndani ya maneno haya kwa njia hii, unaweza kuhisi kana kwamba Nimefanya jambo lisilokuwa kubwa ama Nimenyoosha ufasiri Wangu mbali kiasi. Kama ni hivyo, usijali, hatujamaliza bado.

Hebu tuzungumze kuhusu “Nyoka Anamshawishi Mwanamke.” Nyoka ni nani? (Shetani.) Shetani anashikilia jukumu la foili katika mpango wa usimamizi wa Mungu wa miaka elfu sita, na ni jukumu ambalo hatuwezi kosa kutaja wakati tunaposhiriki utakatifu wa Mungu. Mbona Nasema hivi? Iwapo hujui uovu na upotovu wa Shetani ama asili ya Shetani, basi huna njia ya kumtambua, wala huwezi kujua utakatifu kweli ni nini. Katika mkanganyiko, watu wanaamini

kwamba kile anachofanya Shetani ni chema, kwa sababu wanaishi ndani ya aina hii ya tabia potovu. Bila foili, bila kitu cha kulinganisha nacho, huwezi kujua utakatifu ni nini. Hiyo ndiyo maana lazima Shetani atajwe hapa. Matamko kama hayo si maneno matupu. Kupitia katika maneno na matendo ya Shetani, tutaona jinsi Shetani anavyotenda, jinsi Shetani anavyowapotosha binadamu, na asili na uso wa Shetani ni upi. Basi mwanamke alimwambia nini nyoka? Mwanamke alimweleza nyoka kile Yehova Mungu alikuwa amemwambia. Kwa kufuata alichosema, alikuwa amethibitisha uhalali wa yote ambayo Mungu alikuwa amemwambia? Hangeweza kuthibitisha haya, angeweza? Kama mtu ambaye alikuwa ameumbwa karibuni, hakuwa na uwezo wa kutambua mema kutoka kwa maovu, wala hakuwa na uwezo wa kufahamu chochote karibu naye. Kwa kutathmini maneno aliyomwambia nyoka hakuwa amethibitisha maneno ya Mungu kuwa kweli katika moyo wake; huu ulikuwa mtazamo wake. Hivyo wakati nyoka aliona kwamba mwanamke huyo hakuwa na mtazamo wa uhakika kwa maneno ya Mungu, alisema: “Bila shaka hamtakufa: Kwa kuwa Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, macho yenu yatafunuliwa, nanyi mtakuwa kama miungu, mkijua mema na maovu.” Kuna chochote kibaya na maneno haya? Mlipomaliza kusoma sentensi hii, mlipata hisia ya nia za nyoka? Nyoka ana nia gani? (Kumjaribu mwanadamu kufanya dhambi.) Anataka kumjaribu mwanamke huyu kumfanya aache kusikiza maneno ya Mungu, lakini hakuongea moja kwa moja. Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba ana ujanja sana. Anaonyesha maana yake kwa njia ya udanganyifu na ya kukwepa ili kufikia malengo anayonuia ambayo anaficha kutoka kwa mwanadamu ndani yake—huu ndio ujanja wa nyoka. Shetani amewahi kuzungumza na kutenda hivi. Anasema “sio kwa uhakika,” bila kuthibitisha kwa njia moja au nyingine. Lakini baada ya kusikia haya, moyo wa huyu mwanamke mjinga uliguswa. Nyoka alifurahia kwa sababu maneno yake yalikuwa na matokeo yaliyotarajiwa—hii ilikuwa nia ya ujanja ya Nyoka. Zaidi ya hayo, kwa kuahidi matokeo ambayo mwanadamu aliamini kuwa mema, alimshawishi, akisema, “siku mtakayokula matunda ya mti huo, macho yenu yatafunuliwa.” Hivyo mwanamke anafikiria: “Kufumbuliwa macho yangu ni jambo zuri!” Na kisha akasema kitu kizuri zaidi, maneno yasiyojulikana na mwanadamu, maneno yaliyo na nguvu kubwa ya majaribu juu ya wale wanaoyasikia: “nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na maovu.” Je, maneno haya hayamvutii mwanadamu sana? Ni kama mtu kukwambia: “Uso wako una umbo nzuri. Ni mfupi kidogo katika daraja la pua, lakini ukiirekebisha, utakuwa mrembo wa kupindukia!” Kwa mtu ambaye hajawahi kutaka kufanya upasuaji wa mapambo, moyo wake utaguswa kusikia maneno haya? Je, maneno haya ni ya kushawishi? Ushawishi huu unakuvutia? Ni wa kujaribu? (Ndiyo.) Je, Mungu husema mambo kama haya? Kulikuwa na dokezo lolote la haya katika maneno ya Mungu tuliyoyaangalia sasa hivi? (La.) Je, Mungu husema Anachofikiria katika moyo Wake? Mwanadamu anaweza kuona moyo wa Mungu kupitia maneno Yake? (Ndiyo.) Lakini wakati nyoka alikuwa amesema maneno haya kwa

mwanamke, uliweza kuona moyo wake? (La.) Na kwa sababu ya ujinga wa mwanadamu, mwanadamu alishawishiwa kwa urahisi na maneno ya nyokana alidanganywa kwa urahisi. Hivyo uliweza kuona nia za Shetani? Uliweza kuona madhumuni nyuma ya kile alichosema? Uliweza kuona njama na mpango wake wa ujanja? (La.) Ni aina gani ya tabia inayowakilishwa na njia ya mazungumzo ya Shetani? Ni aina gani ya kiini ulichoona ndani ya Shetani kupitia maneno haya? Je, ni mwenye kudhuru kwa siri? Pengine juujuu anakupa tabasamu ama kutofichua maonyesho yoyote. Lakini katika moyo wake anahesabu jinsi ya kufikia lengo lake, na ni lengo hili ambalo huwezi kuliona. Kisha unashawishiwa na ahadi zote anazokupa, manufaa yote anayozungumzia. Unayaona kuwa mazuri, na unahisi kwamba kile anachosema ni cha kufaa zaidi, kikubwa zaidi kuliko asemacho Mungu. Wakati haya yanafanyika, je, mwanadamu basi hawi mfungwa mtiifu? Je, mbinu hizi zinazotumiwa na Shetani si za kikatili? Unajikubali kuzama chini. Bila ya Shetani kusongeza kidole, kwa sentensi hizi mbili unafurahia kumfuata na kumtii. Lengo lake limefikwa. Nia hii si ya husuda? Huu sio uso wa kimsingi kabisa wa Shetani? Kutoka kwa maneno ya Shetani, mwanadamu anaweza kuona nia zake za husuda, kuona uso wake wenye sura mbaya na kiini chake. Sivyo? Kwa kulinganisha sentensi hizi, bila uchambuzi pengine unaweza kuhisi kana kwamba maneno ya Yehova Mungu ni ya kuchusha, ya kawaida na ya wote, kwamba hayastahili kuhangaikiwa kuusifu uaminifu wa Mungu. Tunapochukua maneno ya Shetani na uso wake wenye sura mbaya na kuvitumia kama foili, hata hivyo, je, haya maneno ya Mungu yanabeba uzito mwingi kwa watu wa leo? (Ndiyo.) Kupitia foili hii, mwanadamu anaweza kuhisi kutokuwa na dosari kwa Mungu. Kila neno analosema Shetani pamoja na nia zake, malengo yake na jinsi anavyoongea—yote yamepotoshwa. Ni nini sifa muhimu ya njia yake ya kuzungumza? Anatomia maneno yasiyo dhahiri kukushawishi bila kukuruhusu kumwona, wala hakuruhusu kutambua lengo lake ni nini; anakuacha uchukue chambo, akikufanya umsifu na kuimba uzuri wake. Hii siyo hila ya daima ya Shetani? (Ndiyo.) Hebu sasa tuangalie maneno na maonyesho mengine ya Shetani yanayomruhusu mwanadamu kuona uso wake wenye sura mbaya. Hebu tuendeleo kusoma baadhi ya maandiko.

Mazungumzo kati ya Shetani na Yehova Mungu

Ayubu 1:6-11 Sasa kulikuweco na siku ambapo wana wa Mungu walikuja kujidhihirisha mbele za Yehova, naye Shetani akaja pia kati yao. Naye Yehova akasema kwa Shetani, Ni wapi umetoka? Basi Shetani akamjibu Yehova, na kunena, Natoka katika kuenda hapa na pale duniani, na katika kutembea juu chini humo. Naye Yehova akasema kwa Shetani, je, umemfikiria mtumishi Wangu Ayubu, kwamba hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu? Kisha Shetani akamjibu Yehova, na kusema, je, Ayubu anamcha Mungu bure? Wewe hujamzunguka kila upande na ukingo, na kila upande wa nyumba yake, na kila upande wa yote aliyo nayo? Umebariki kazi ya

mikono yake, na mali yake inaongezeka nchini. Lakini nyosha mbele mkono Wako sasa, na uguse yote aliyo nayo, na yeye atakulaani mbele ya uso Wako.

Ayubu 2:1-5 Tena kulikuweco na siku ambapo wana wa Mungu walikuja kujidhihirisha mbele za Yehova, naye Shetani akaja pia kati yao ili kujidhihirisha mbele za Yehova. Naye Yehova akasema kwa Shetani, Ni wapi umetoka? Na Shetani akamjibu Yehova, na kunena, Natoka katika kuenda hapa na pale duniani, na katika kutembea juu chini humo. Naye Yehova akasema kwa Shetani, je, umemfikiria mtumishi Wangu Ayubu, kwamba hakuna hata mtu kama yeye duniani, mtu mtimilifu na mwaminifu, ambaye anamcha Mungu, na kuepuka maovu? Na bado anashikilia ukamilifu wake, ingawa ulinichochea dhidi yake, ili mimi nimwangamize bila sababu. Naye Shetani akamjibu Yehova, na akasema, Ngozi kwa ngozi, ndiyo, yote ambayo mtu anayo atayatoa kwa sababu ya uhai wake. Lakini nyosha mbele mkono Wako sasa, na uguse mfupa wake na nyama yake, na yeye atakulaani mbele ya uso Wako.

Vifungu hivi viwili vinajumuisha kikamilifu mazungumzo kati ya Mungu na Shetani; vinarekodi kile alichosema Mungu na kile alichosema Shetani. Mungu hakuzungumza sana, na Aliongea kwa urahisi sana. Tunaweza kuona utakatifu wa Mungu katika maneno rahisi ya Mungu? Wengine watasema “hii si rahisi.” Hivyo tunaweza kuona ubaya wa Shetani katika majibu yake? (Ndiyo.) Kwanza wacha tuangalie ni aina gani ya swali ambalo Yehova Mungu alimwuliza Shetani. “Ni wapi umetoka?” Hili ni swali linaloeleweka kwa urahisi? Kuna maana iliyofichwa? (La.) Ni swali tu, safi, bila madhumuni mengine. Kama Ngingekuuliza: “Unatoka wapi wewe?” mngejibu vipi? Ni swali gumu kujibu? Mngesema: “Natoka katika kuzungukazunguka, na katika kutembea huku na huku?” (La.) Hamngejibu namna hii, kwa hivyo mnahisi aje mnapomwona Shetani akijibu kwa njia hii? (Tunahisi kwamba Shetani ni mpumbavu na mjanja.) Unaweza kusema ni nini Ninachohisi? Kila wakati Ninapoona maneno haya Nahisi kuchukizwa kwa sababu anazungumza bila kusema lolote. Alijibu swali la Mungu? Maneno yake hayakuwa jibu, hakukuwa na matokeo yoyote. Hayakuwa jibu lililoelekezwa kwa swali la Mungu. “Natoka katika kuenda hapa na pale duniani, na katika kutembea juu chini humo.” Unaelewa nini kutoka kwa maneno haya? Shetani ametoka wapi duniani? Mmepata jibu? (La.) Hii ndiyo “akili” ya ujanja wa Shetani, kutomwacha yeyote kujua anachosema. Baada ya kuyasikia maneno haya, bado huwezi kutambua ni nini amesema, ilhali amemaliza kujibu. Anaamini kwamba amejibu vizuri sana. Basi unahisi vipi? Kuchukizwa? (Ndiyo.) Sasa unaanza kuchukizwa na maneno haya, Shetani haongei moja kwa moja, hivyo kukuacha ukikuna kichwa chako na kutoweza kutambua chanzo cha maneno yake. Wakati mwingine anazungumza kimakusudi, na wakati mwingine anatawaliwa na kiini chake mwenyewe, asili yake. Maneno haya yalitoka moja kwa moja kinywani mwa Shetani. Hayakuzingatiwa kwa muda mrefu na kisha kuzungumzwa na Shetani, akijifikiri mwenyewe mwerevu; aliyaeleza kiasili. Punde tu

unapomuuliza anatoka wapi, anatumia maneno haya kukujibu. Unahisi kuchanganyikiwa, bila kujua ametoka wapi hasa. Kuna wowote kati yenu wanaozungumza hivi? (Ndiyo.) Hii ni njia ya aina gani ya kuzungumza? (Si dhahiri na haina jibu la uhakika.) Tunapaswa kutumia aina gani ya maneno kuelezea namna hii ya kuzungumza? Ni ya kupotosha na kudanganya, siyo? Tuseme mtu hataki wengine wajue alipoenda jana. Unawauliza: “Nilikuona jana. Ulikuwa unaelekea wapi?” Hawakujibu moja kwa moja kusema mahali walienda jana. Wanasema “Jana ilikuwa siku kweli. Nimechoka sana!” Je, walijibu swali lako? Walijibu, lakini hilo si jibu ulilokuwa unataka. Hii ni “akili” ya ujanja wa mwanadamu. Huwezi kugundua wanachomaanisha ama kutambua chanzo ama nia nyuma ya maneno yao. Hujui ni nini wanachojaribu kuepuka kwa sababu ndani ya mioyo yao wanayo hadithi yao wenyewe—hii ni yenye kudhuru kwa siri. Je, ninyi pia huongea hivi mara nyingi? (Ndiyo.) Basi madhumuni yenu ni yapi? Je, huwa ni kulinda maslahi yenu wakati mwingine, kudumisha nafasi yenu wakati mwingine, taswira yenu, kuweka siri za maisha yenu ya kibinafsi, kuokoa sifa zenu binafsi? Licha ya madhumuni, hayatenganishwi na maslahi yenu, yanahusiana na maslahi yenu. Hii sio asili ya mwanadamu? Si kila mtu aliye na asili ya aina hii ni kama Shetani? Tunaweza kusema hivi, sivyo? Kuzungumza kwa ujumla, huu udhihirisho ni wenye makuruhu na wa kusinya. Mnahisi pia sasa kuchukizwa, sivyo? (Ndiyo.)

Tukiangalia tena kifungu cha kwanza, Shetani anamjibu tena Yehova, akisema: “Je, Ayubu anamcha Mungu bure?” Shetani anaanzisha mashambulizi juu ya tathmini ya Yehova kwa Ayubu, na shambulio hili linapakwa rangi na uhasama. “Wewe hujamzunguka kila upande na ukingo, na kila upande wa nyumba yake, na kila upande wa yote aliyo nayo?” Huu ndio uelewa na tathmini ya Shetani ya kazi ya Yehova kwa Ayubu. Shetani anaitathmini hivi, akisema: “Umebariki kazi ya mikono yake, na mali yake inaongezeka nchini. Lakini nyosha mbele mkono Wako sasa, na uguse yote aliyo nayo, na yeye atakulaani mbele ya uso Wako.” Shetani huongea kwa utata kila mara, lakini hapa anaongea kwa uhakika. Hata hivyo, maneno haya yaliyozungumzwa kwa uhakika ni shambulio, ni kufuru na ni upinzani kwa Yehova Mungu, kwa Mungu Mwenyewe. Mnahisi vipi mnapomsikia? Mnahisi chuki? Mnaaweza kuona nia zake? Kwanza kabisa, anakataa kabisa tathmini ya Yehova ya Ayubu—yule anayemwogopa Mungu na kuepuka maovu. Kisha anakataa kabisa kila kitu anachosema na kufanya Ayubu, yaani, anakataa kumcha Yehova. Je, yeye anashitaki? Shetani anashitaki, anakataa na anashuku kila anachofanya na kusema Yehova. Haamini, akisema, “Ukisema mambo yako namna hii, mbona sijaiona? Umempa baraka nyingi, anawezaje kukosa kukucha?” Je, huku si kukataa kabisa kila anachofanya Mungu? Kushitaki, kukataa, kufuru—maneno yake si ya ugomvi? Si ni maonyesho ya ukweli ya kile anachofikiria Shetani ndani ya moyo wake? Haya maneno hakika si sawa na maneno tuliyoayasoma hivi sasa: “Natoka katika kuenda hapa na pale duniani, na katika kutembea juu chini humo.” Ni tofauti sana na hayo. Kupitia maneno haya, Shetani anaweka wazi mtazamo

wake kwa Mungu na kuchukizwa na kumcha Mungu kwa Ayubu ambako kuko katika moyo wake. Haya yakifanyika, ubaya wake na asili yake mbovu inafichuliwa kabisa. Anawachukia wale wanaomcha Mungu, anawachukia wale wanaoepukana na maovu, na hata zaidi anamchukia Yehova kwa sababu ya kumpa mwanadamu baraka. Anataka kutumia fursa hii kumwangamiza Ayubu ambaye Mungu alimwinua na mkono Wake mwenyewe, kumwangamiza, akisema: “Unasema Ayubu anakuogopa na kuepukana na maovu. Naiona vingine.” Anatumia mbinu mbalimbali kumchochea na kumjaribu Yehova, na kutumia mbinu mbalimbali ili Yehova Mungu amkabidhi Ayubu kwa Shetani ili atawaliwe, adhuriwe na ashughulikiwe kwa ukatili. Anataka kutumia fursa hii ili kumwangamiza mtu huyu ambaye ni mwenye haki na mtimilifu katika macho ya Mungu. Yeye kuwa na moyo wa aina hii ni msukumo wa muda mfupi? La, siyo. Imekuwa ikiundwa kwa muda mrefu. Mungu anafanya kazi, Mungu anamtunza mtu, anamwangalia mtu, na Shetani anafuata hatua Yake yote. Yeyote anayefadhiliwa na Mungu, Shetani pia anatazama, akifuata nyuma. Iwapo Mungu anamtaka mtu huyu, Shetani atafanya kila kitu kwa uwezo wake kumzuia Mungu, akitumia mbinu mbalimbali mbovu kujaribu, kusumbua na kuharibu kazi anayofanya Mungu ili kufikia lengo lake lililofichwa. Lengo lake ni nini? Hataki Mungu awe na mtu yeyote; anataka wale wote ambao Mungu anataka, kuwamiliki, kuwatawala, kuwaelekeza ili wamwabudu, ili watende maovu pamoja naye. Je, hii siyo nia ya husuda ya Shetani? Kwa kawaida, ninyi husema mara nyingi kwamba Shetani ni mwovu sana, mbaya sana, lakini umemwona? Mnaweza kuona tu jinsi ambavyo mwanadamu ni mbaya na hamjaona kwa uhakika jinsi ambavyo Shetani ni mbaya sana. Lakini mmemwona kwa hili swala linalohusiana na Ayubu? (Ndiyo.) Swala hili limeufanya uso wenye sura mbaya wa Shetani na kiini chake kuwa wazi kabisa. Shetani yuko vitani na Mungu, akifuata nyuma Yake. Lengo lake ni kubomoa kazi yote ambayo Mungu anataka Kufanya, kuwamiliki na kudhibiti wale wote ambao Mungu anawataka, kuwafisha kabisa wale ambao Mungu anataka. Kama hawajafishwa, basi wanakuja kwa milki ya Shetani kutumiwa naye—hili ndilo lengo lake. Na Mungu anafanya nini? Mungu anasema tu sentensi rahisi katika kifungu hiki; hakuna rekodi ya chochote zaidi ambacho Mungu anafanya, lakini tunaona kwamba kuna rekodi nyingi zaidi za kile ambacho Shetani anafanya na kusema. Katika kifungu cha maandishi hapa chini, Yehova alimwuliza Shetani, “Ni wapi umetoka?” Jibu la Shetani ni nini? (Bado ni “Natoka katika kuenda hapa na pale duniani, na katika kutembea juu chini humo.”) Bado ni sentensi hiyo. Imekuwaje wito wa Shetani, kazi ya Shetani ya ujuzi wa juu? Si Shetani ni wa kuchukia? Kusema sentensi hii inayochafua moyo mara moja inatosha. Kwa nini Shetani daima anarejelea Sentensi hii? Hii inadhihirisha kitu kimoja: asili ya Shetani haibadiliki. Shetani hawezi kutumia visingizio kuficha uso wake mbaya. Mungu anamwuliza swali na anajibu kwa njia kama hiyo, sembuse anavyotendea watu! Hamwogopi Mungu, hamchi Mungu, na hamtii Mungu. Hivyo anathubutu kuwa na kiburi kwa ukaidi mbele ya Mungu, kutumia haya maneno ili kujaribu kupuuza swali la

Mungu, kutumia jibu hili moja kwa kurudia rudia kujibu swali la Mungu, kujaribu kutumia jibu hili kumshangaza Mungu—huu ndio uso usiopendeza wa Shetani. Haamini uweza wa Mungu, haamini mamlaka ya Mungu, na hakika hayuko tayari kujinyenyekeza chini ya mamlaka ya Mungu. Daima anampinga Mungu, daima anashambulia yote anayofanya Mungu, akijaribu kuharibu yote ambayo Mungu anafanya—hili ndilo lengo lake ovu.

Katika mpango wa Mungu wa usimamizi wa miaka elfu sita, vifungu hivi viwili ambavyo Shetani anasema na mambo ambayo Shetani anafanya katika kitabu cha Ayubu yanawakilisha upinzani wake kwa Mungu, na hivi ndivyo Shetani akidhihirisha alivyo kwa kweli. Umeyaona maneno na matendo ya Shetani katika maisha halisi? Utakapoyaona, unaweza kutoyafikiria kuwa vitu vilivyoongelewa na Shetani, lakini badala yake kuyafikiria kuwa vitu vilivyoongelewa na mwanadamu. Kipi kilichowakilishwa, wakati mambo kama hayo yanazungumzwa na mwanadamu? Shetani anawakilishwa? Hata kama utamtambua, bado huwezi kuona kwamba ukweli unazungumzwa na Shetani. Lakini hapa na sasa umeona bila shaka kile ambacho Shetani mwenyewe amesema. Sasa una uelewa usio na shaka na ulio wazi kabisa wa uso wenye sura mbaya na uovu wa Shetani. Hivyo hivi vifungu viwili vilivyozungumzwa na Shetani ni vya thamani kwa watu wa leo kuweza kujua asili ya Shetani? Hivi vifungu viwili vinastahili kukusanywa ili binadamu leo aweze kutambua uso wenye sura mbaya wa Shetani, kutambua uso wa asili na wa kweli wa Shetani? Ingawa kusema jambo hili hakuonekani kufaa sana, kulieleza kwa njia hii bado kunaweza kuchukuliwa kuwa sahihi. Naweza tu kuliweka kwa njia hii na iwapo mnalielewa, basi imetosha. Tena na tena, Shetani anayashambulia mambo ambayo Yehova anafanya, akitoa mashtaka kuhusu kumcha Yehova kwa Ayubu. Anajaribu kumchochea Yehova kwa kutumia mbinu mbalimbali, kumfanya Yehova Mungu kumkubali kumjaribu Ayubu. Maneno yake basi yanachochea sana. Basi Niambieni, baada ya Shetani kuzungumza maneno haya, Mungu anaweza kuona wazi kile ambacho Shetani anataka kufanya? (Ndiyo.) Katika moyo wa Mungu, huyu mtu Ayubu ambaye Mungu anamwangalia—huyu mtumishi wa Mungu, ambaye Mungu anamchukulia kuwa mwenye haki, mtu mtimilifu—anaweza kuyahimili majaribio ya aina hii? (Ndiyo.) Kwa nini Mungu ana uhakika sana kuhusu hilo? Mungu huchunguza moyo wa binadamu daima? (Ndiyo.) Kwa hivyo Shetani anaweza kuchunguza moyo wa binadamu? Shetani hawezi. Hata kama Shetani anaweza kuona moyo wa mwanadamu, asili yake mbovu haiwezi kuamini kwamba utakatifu ni utakatifu, ama kwamba uchafu ni uchafu. Shetani mwovu hawezi kuthamini chochote kilicho takatifu, chenye haki ama chenye kung’aa. Shetani hawezi kuepuka kuumiza kwa kutenda kupitia asili yake, uovu wake, na kupitia mbinu hizi anazotumia. Hata kwa hatari ya yeye kuadhibiwa na kuangamizwa na Mungu, hasiti kumpinga Mungu kwa ukaidi—huu ni uovu, hii ni asili ya Shetani. Kwa hivyo katika kifungu hiki, Shetani anasema: “Ngozi kwa ngozi, ndiyo, yote ambayo mtu anayo atayatoa kwa sababu

ya uhai wake. Lakini nyosha mbele mkono wako sasa, na uguse mfupa wake na nyama yake, na yeye atakulaani mbele ya uso Wako.” Shetani anafikiri kwamba kumcha Mungu kwa mwanadamu ni kwa sababu mwanadamu amepata manufaa mengi kutoka kwa Mungu. Mwanadamu hupata manufaa mengi kutoka kwa Mungu, kwa hivyo anasema Mungu ni mwema. Lakini si kwa sababu Mungu ni mwema, ni kwa sababu tu mwanadamu amepata manufaa mengi na hivyo anaweza kumcha Mungu kwa njia hii: Punde Mungu anapomnyima manufaa haya, basi anaachana na Mungu. Katika asili yake mbovu, Shetani haamini kwamba moyo wa mwanadamu kwa kweli unaweza kumcha Mungu. Kwa sababu ya asili yake mbovu hajui utakatifu ni nini, na hata chini zaidi hajui heshima ya kuogopa ni nini. Hajui ni nini kumtii Mungu ama ni nini kumcha Mungu. Kwa sababu yeye mwenyewe hazijui, anafikiri mwanadamu hawezi kumcha Mungu pia. Niambieni, si Shetani ni mwovu? Isipokuwa kanisa letu, hakuna kati ya makundi ya kidini na madhehebu mbalimbali, ama makundi ya kidini na ya kijamii, yanayoamini uwepo wa Mungu, sembuse wao kuamini kwamba Mungu amekuwa mwili na Anafanya kazi ya hukumu, hivyo wanafikiri kwamba kile unachoamini si Mungu. Mwanamume mzinzi huangalia huku na kule na kumwona kila mtu mwingine kama mzinzi, kama alivyo yeye. Mwanadamu anayedanganya kila wakati anaangalia na kuona hakuna mtu mwaminifu, anawaona wote wakidanganya. Mtu mwovu anawaona watu wote wakiwa waovu na anataka kupigana na kila mtu anayemwona. Wakati wale watu ambao walio na uaminifu kwa kulinganisha wanawaona wote kuwa waaminifu, na hivyo daima wanalaghaiwa, wanadanganywa, na hakuna wanachoweza kufanya kuhusu hilo. Nasema mifano hii michache ili kuwafanya kuwa na uhakika zaidi: asili mbovu ya Shetani si msukumo wa muda mfupi ama kitu kinachosababishwa na mazingira yake, wala si udhihirisho wa muda ulioletwa na sababu yoyote ama usuli wowote. Sivyo kabisa! Hana namna ila kuwa hivyo! Hawezi kufanya chochote chema! Hata anaposema kitu kinachofurahisha kusikia, anakushawishi tu. Kadiri maneno yake yanavyofurahisha, yenye busara zaidi, uungwana zaidi, ndivyo nia zake za husuda zinakuwa za kijicho zaidi nyuma ya maneno haya. Shetani anaonyesha uso na asili ya aina gani katika vifungu hivi viwili? (Ya kudhuru kwa siri, yenye kijicho, na mbovu.) Tabia yake ya msingi ni mbovu, hasa mbovu na yenye kijicho.

Kwa sababu sasa tumemaliza kuzungumza kuhusu Shetani, hebu turudie kuzungumza kuhusu Mungu wetu. Wakati wa mpango wa usimamizi wa miaka elfu sita wa Mungu, matamshi machache sana ya moja kwa moja ya Mungu yamerekodiwa katika Biblia, na yale yaliyorekodiwa ni rahisi sana. Hivyo acha tuanzia mwanzoni. Mungu alimuumba mwanadamu na tangu hapo daima Ameongoza maisha ya binadamu. Iwe kwa kuwapa wanadamu baraka, kuwapa sheria na amri Zake, ama kuweka masharti kanuni mbalimbali za maisha, mnajua lengo analoniua Mungu kwa kufanya mambo haya ni nini? Kwanza, mnaweza kusema kwa uhakika

kwamba yote anayofanya Mungu ni kwa wema wa binadamu? Mnaweza kufikiria kwamba sentensi hii kwa kulinganishwa ni pana na tupu, lakini kuzungumza hasa, si kila kitu anachofanya Mungu ni cha kumwongoza na kumwelekeza mwanadamu kuishi maisha ya kawaida? Iwe ili mwanadamu ashike kanuni Zake ama ashike sheria Zake, lengo la Mungu ni kwa mwanadamu kutomwabudu Shetani, kutodhuriwa na Shetani; hili ndilo la msingi zaidi, na hili ndilo lililofanywa mwanzoni kabisa. Mwanzoni kabisa, wakati mwanadamu hakuelewa mapenzi ya Mungu, Alichukua baadhi ya sheria na kanuni rahisi na kuweka masharti yaliyoshughulikia vipengele vyote vinavyoweza kufikiwa. Masharti haya ni rahisi, lakini ndani yake kuna mapenzi ya Mungu. Mungu anamthamini, Anamtunza na kwa hakika Anampenda mwanadamu. Sivyo? (Ndiyo.) Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba moyo Wake ni mtakatifu? Tunaweza kusema kwamba moyo wake ni safi? (Ndiyo.) Je, Mungu anazo nia zilizofichwa? (La.) Kwa hivyo hili lengo Lake ni sahihi na halisi? (Ndiyo.) Haijalishi masharti aliyoweka Mungu, katika kazi Yake yote yana athari halisi kwa mwanadamu, na yanaongoza njia. Kwa hivyo kuna fikira zozote za kibinafsi katika akili ya Mungu? Je, Mungu anayo malengo zaidi kuhusiana na mwanadamu, ama Anataka kumtumia mwanadamu kwa jinsi fulani? (La.) Sivyo hata kidogo. Mungu anafanya Asemavyo, na pia Anafikiria namna hii moyoni Mwake. Hakuna mchanganyiko wa madhumuni, hakuna fikira za kibinafsi. Hajifanyii chochote, lakini Anamfanyia mwanadamu kila kitu kabisa, bila malengo yoyote ya kibinafsi. Ingawa Ana mipango na nia kwa mwanadamu, Hajifanyii chochote. Kila kitu Anachofanya kinafanyiwa mwanadamu tu, kumlinda mwanadamu, kumhifadhi mwanadamu dhidi ya kupotezwa. Hivyo si moyo huu Wake ni wenye thamani? Unaweza kuona hata ishara kidogo zaidi ya moyo wenye thamani kama huu ndani ya Shetani? (La.) Hamuwezi kuliona dokezo moja la moyo huu kwa Shetani. Kila kitu anachofanya Mungu kinafichuliwa kiasili. Sasa, angalia jinsi ambavyo Mungu anafanya kazi; Anafanyaje kazi kazi Yake? Je, Mungu anazichukua sheria hizi na maneno Yake na kuyafunga pamoja kwa kukaza juu ya kichwa cha kila mtu, kama kama laana inayofungwa na ukanda^[a], Akizilazimisha kwa kila mwanadamu? Je, Anafanya kazi namna hii? (La.) Kwa hivyo Mungu anafanya kazi Yake namna gani? (Anatuongoza. Anatupa mawaidha na kututia moyo.) Je, Anatishia? Je, Anawazungumzia kwa njia inayochanganya? (La.) Wakati huelewi ukweli, Mungu hukuongoza vipi? (Yeye huangaza mwangaza.) Anaangaza mwangaza kwako, akikwambia wazi kwamba haya hayaambatani na ukweli, na kile unachofaa kufanya. Kutoka kwa njia hizi ambazo Mungu anafanya kazi, unahisi kwamba una uhusiano wa aina gani na Mungu? Zinakufanya uhisi kwamba Mungu yuko mbali na ufahamu wako? (La.) Hivyo zinakufanya uhisi vipi? Mungu yuko hasa karibu na wewe, hakuna umbali kati yenu. Wakati Mungu anakuongoza, Anapokukimu, Anapokusaidia na kukufadhili, unahisi urafiki wa Mungu, kuheshimika Kwake, unahisi jinsi Anavyopendeza, jinsi Alivyo mwema. Lakini Mungu anaposhutumu upotovu wako, ama Anapokuhukumu na kukufundisha nidhamu kwa sababu ya

kuasi dhidi Yake, Mungu anatumia njia gani? Anakushutumu kwa kutumia maneno? Anakufundisha nidhamu kupitia mazingira yako na kupitia kwa watu, masuala na mambo? (Ndiyo.) Nidhamu hii inafika kiwango kipi? Je, inafikia mahali sawa ambapo Shetani anamduru mwanadamu? (La, inafika kiwango ambacho mwanadamu anaweza kuvumilia.) Mungu anafanya kazi kwa njia ya upole, laini, yenye upendo na ya kujali, kwa njia iliyopimwa kwa namna ya ajabu na sahihi. Njia Yake haikufanyi uhisi hisia kali ya mhemuko kama vile; “Mungu lazima aniache nifanye hivi” ama “Lazima Mungu aniache nifanye vile.” Mungu kamwe hakupi mawazo makali ya aina hiyo ama hisia kali zinazofanya mambo kutovumilika. Sivyo? Hata unapoyakubali maneno ya Mungu ya hukumu na kuadibu, unahisi vipi basi? Unapohisi mamlaka ya Mungu na nguvu ya Mungu, unahisi vipi basi? Unahisi kwamba Mungu ni mtakatifu na asiyekosewa? (Ndiyo.) Unahisi ukiwa mbali na Mungu nyakati hizi? Unahisi unamwogopa Mungu? La, badala yake, unahisi heshima inayomcha Mungu. Je, watu hawahisi haya mambo yote kwa sababu ya kazi ya Mungu? Wangukuwa na hisia hizi iwapo Shetani angefanya kazi kwa mwanadamu? (La.) Mungu hutumia maneno Yake, ukweli Wake na uhai Wake kuendelea bila kusita kumkimu mwanadamu, kumfadhili mwanadamu. Wakati mwanadamu ni mnyonge, wakati mwanadamu anahisi huzuni, Mungu kwa hakika hazungumzi kwa ukali, akisema: “Usihisi mwenye kukata tamaa? Kwa nini wewe ni dhaifu? Kuna sababu gani ya kuwa dhaifu? Wewe huwa dhaifu sana daima, na wewe daima huwa hasi! Kuna haja gani ya wewe kuwa hai? Kufa tu!” Je, Mungu anafanya kazi hivi? (La.) Je, Mungu ana mamlaka ya kutenda namna hii? (Ndiyo.) Lakini Mungu hatendi kwa namna hii. Mungu hatendi hivi kwa sababu ya kiini Chake, kiini cha utakatifu wa Mungu. Upendo Wake kwa mwanadamu, kuthamini na utunzaji Wake wa mwanadamu haviwezi kuelezwa wazi kwa sentensi moja au mbili. Si kitu kinacholetwa na kujisifu kwa mwanadamu lakini ni kitu ambacho Mungu analeta kupitia kwa vitendo halisi; ni ufunuo wa kiini cha Mungu. Je, hizi njia zote ambazo Mungu anafanya kazi zinaweza kumruhusu mwanadamu kuona utakatifu wa Mungu? Kwa hizi njia zote ambazo Mungu anafanya kazi, zikiwemo nia nzuri za Mungu, zikiwemo athari ambazo Mungu anataka kutimiza kwa mwanadamu, zikiwemo njia mbalimbali ambazo Mungu anatumia kufanya kazi kwa mwanadamu, aina ya kazi Anayofanya, kile Anachotaka mwanadamu kuelewa—umeona uovu ama ujanja wowote katika nia nzuri za Mungu? (La.) Hivyo, katika kila kitu ambacho Mungu anafanya, kila kitu ambacho Mungu anasema, kila kitu anachofikiria katika moyo Wake, na pia kiini chote cha Mungu anachofichua—tunaweza kumwita Mungu mtakatifu? (Ndiyo.) Mwanadamu yeyote amewahi kuona utakatifu huu duniani, ama kwake mwenyewe? Mbali na Mungu, umewahi kuuona ndani ya mtu yeyote ama ndani Shetani? (La.) Kutoka kwa yale tuliyoyazungumzia hadi sasa, tunaweza kumwita Mungu wa kipekee, Mungu mtakatifu Mwenyewe? (Ndiyo.) Yote ambayo Mungu anampa mwanadamu, yakiwemo maneno ya Mungu, njia tofauti ambazo kwazo Mungu anafanya kazi kwa mwanadamu, kile ambacho Mungu

anamwambia mwanadamu, kile ambacho Mungu anamkumbusha mwanadamu kuhusu, kile ambacho Anashauri na kutia moyo, vyote vimetoka kwa kiini kimoja: Vyote vimetoka kwa utakatifu wa Mungu. Iwapo hakungekuwa na Mungu mtakatifu kama huyu, hakuna mwanadamu ambaye angechukua nafasi Yake kufanya kazi Anayofanya. Iwapo Mungu angewachukua watu hawa na kuwakabidhi kabisa kwa Shetani, mmewahi kuzingatia mngekuwa katika hali ya aina gani leo? Nyinyi nyote mngekuwa mmeketi hapa, kamili na wasioharibika? Pia mngesema: “Natoka katika kuenda hapa na pale duniani, na katika kutembea juu chini humo”? Mngejitamba hivyo, kutokuwa na haya kabisa na kujigamba bila haya mbele ya Mungu, na kuenda dalji mkizungumza kwa njia kama hiyo? (Ndiyo.) Mngeweza kwa asilimia mia moja! Mngeweza kabisa! Mtazamo wa Shetani kwa mwanadamu unawaruhusu kuona kwamba asili na kiini cha Shetani ni tofauti kabisa na cha Mungu. Kiini kipi cha Shetani ni kinyume cha utakatifu wa Mungu? (Uovu wake.) Asili ya uovu ya Shetani ni kinyume na utakatifu wa Mungu. Watu wengi zaidi hawatambui maonyesho haya ya Mungu na kiini hiki cha utakatifu wa Mungu ni kwa sababu wanaishi chini ya umiliki wa Shetani, ndani ya upotovu wa Shetani na ndani ya boma anamoishi Shetani. Hawajui utakatifu ni nini ama jinsi ya kufafanua utakatifu. Hata unapooni utakatifu wa Mungu, bado huwezi kuufafanua kuwa utakatifu wa Mungu kwa uhakika wowote. Hii ni tofauti katika maarifa ya mwanadamu ya utakatifu wa Mungu.

Ni sifa ya uwakilishi ya aina gani inayoonyeshwa na kazi ya Shetani kwa mwanadamu? Mnapaswa kuweza kujifunza hii kupitia uzoefu wenu wenyewe—ndiyo sifa ya uwakilishi zaidi ya Shetani, kitu ambacho anafanya zaidi, kitu ambacho anajaribu kufanya na kila mtu. Pengine hamwezi kuona sifa hii, kwa hivyo hamhisi kwamba Shetani ni wa kutisha na wa kuchukia sana. Kuna mtu anayejua sifa hii ni nini? (Kila kitu anachofanya, anafanya ili kumdhuru mwanadamu.) Anamdhuru mwanadamu vipi? Mnaweza kuniambia hasa zaidi na kwa kina? (Anamshawishi, anamlaghai na kumjaribu mwanadamu.) Hii ni sahihi, hii inaonyesha vipengele kadhaa. Pia anamdanganya kumshambulia na kumtuhumu mwanadamu—haya yote. Kuna mengine zaidi? (Anasema uwongo.) Udanganyifu na uongo hujitokeza kiasili kabisa kwa Shetani. Anafanya hivi mara nyingi hadi uongo unabubujika kutoka kwa mdomo wake bila yeye hata kuhitaji kufikiria. Mengine zaidi? (Anapanda mfarakano.) Hii si muhimu sana. Nitawaelezea kitu ambacho kitawatisha, lakini Sifanyi hivyo ili kuwaogopesha. Mungu anafanya kazi kwa mwanadamu na mwanadamu anathaminiwa katika mtazamo wa Mungu na moyo Wake. Kinyume na hayo, je, Shetani anamthamini mwanadamu? Hamthamini mwanadamu. Anachofikiria tu ni kumdhuru mwanadamu. Hii si sahihi? Wakati anafikiria kumdhuru mwanadamu, anafanya hivyo katika hali ya dharura ya akili? (Ndiyo.) Kwa hivyo inapokuja kwa kazi ya Shetani kwa mwanadamu, hapa Nina virai viwili vinayoweza kuelezea vizuri asili yenye nia mbaya na ovu ya Shetani, vinavyoweza kuwaruhusu kujua chuki ya Shetani: Katika mtazamo wa Shetani kwa

mwanadamu, daima anataka kumiliki na kumtawala kwa nguvu, kila mmoja wao, ili aweze kufika mahali ambapo anaweza kumdhibiti mwanadamu kabisa, kumdhuru mwanadamu, ili aweze kutimiza lengo hili na tamaa isiyowezekana. “Umiliki wa nguvu” unamaanisha nini? Unafanyika na kibali chako, ama bila kibali chako? Unafanyika na kujua kwako, ama bila kujua kwako? Ni bila kujua kwako kabisa! Katika hali ambazo huna ufahamu, pengine wakati hajasema chochote ama pengine wakati hajafanya chochote, wakati hakuna kauli kigezo, hakuna muktadha, yuko hapo karibu nawe, akikuzunguka. Anatafuta fursa ya kukunyonya, kisha anakumiliki kwa nguvu, anakutawala, akitimiza lengo lake la kukudhibiti kikamilifu na kukudhuru. Hii ni nia na tabia ya kawaida zaidi katika mapambano ya Shetani dhidi ya Mungu kwa ajili ya mwanadamu. Mnahisi vipi mnaposikia haya? (Tuna hofu na woga katika mioyo yetu.) Mnahisi kuchukizwa? (Ndiyo.) Mnapohisi kuchukizwa, mnafikiria Shetani hana haya? Mnapofikiria Shetani hana haya, mnahisi kuchukizwa na wale watu walio karibu nanyi ambao daima wanataka kuwatawala, wale walio na matarajio yasiyowezekana ya hadhi na maslahi yao? (Ndiyo.) Hivyo ni mbinu gani anazotumia Shetani kumtawala kwa nguvu na kumiliki mwanadamu? Mnaelewa hili vizuri? Mnaposikia maneno haya mawili “umiliki wa nguvu” na “utawala,” mnahisi chukizo na maweza kuhisi uovu ulio katika maneno haya. Bila kibali ama maarifa yako, Shetani anakutawala, anakumiliki kwa nguvu, na kukupotosha. Unaweza kuonja nini kwa moyo wako? Je, unahisi chuki na maudhi? (Ndiyo.) Wakati unahisi hii chuki na maudhi kwa njia hii ya Shetani, una hisia gani kwa Mungu? (Shukrani.) Shukrani kwa Mungu kwa kukuokoa. Kwa hivyo sasa, wakati huu, unayo hamu ama matakwa ya kumwacha Mungu aongoze kila kitu chako na kutawala kila kitu chako? (Ndiyo.) Kwa muktadha upi? Unasema ndiyo kwa sababu unaogopa kumilikiwa kwa nguvu na kutawaliwa na Shetani? (Ndiyo.) Huwezi kuwa na mawazo kama haya, siyo sahihi. Usiwe na hofu, Mungu yuko hapa. Hakuna chochote cha kuhofia. Ukishaelewa asili mbovu ya Shetani, unapaswa kuwa na uelewa sahihi zaidi ama upendo wa kina wa mapenzi ya Mungu, nia nzuri za Mungu, huruma ya Mungu na stahamala kwa mwanadamu na tabia Yake ya haki. Shetani ni wa kuchukia sana, lakini ikiwa hili bado haliutii moyo upendo wako kwa Mungu na utegemezi na uaminifu wako kwa Mungu, basi wewe ni mtu wa aina gani? Uko tayari kumwacha Shetani akudhuru hivyo? Baada ya kuona uovu na ubaya wa Shetani, tunageuka na kisha kumwangalia Mungu. Maarifa yako ya Mungu sasa yamepitia mabadiliko yoyote? Tunaweza kusema Mungu ni mtakatifu? Tunaweza kusema Mungu hana dosari? “Mungu ni utakatifu wa kipekee”—Mungu anaweza kuvumilia jina hili? (Ndiyo.) Hivyo duniani na miongoni mwa mambo yote, ni Mungu Mwenyewe pekee anayeweza kuvumilia huu uelewa wa mwanadamu? Kuna wengine? (La.) Hivyo, ni nini hasa ambacho Mungu anampa mwanadamu? Je, Anakupa tu utunzaji mdogo, wasiwasi na kukutia maanani kidogo wakati huko makini? Mungu amempa nini mwanadamu? Mungu amempa mwanadamu uhai, Amempa mwanadamu kila kitu, na amempa mwanadamu bila masharti bila kudai

chochote, bila nia zozote za siri. Anatumia ukweli, Anatumia maneno Yake, Anatumia uhai Wake kumwongoza na kumwelekeza mwanadamu, kumtoa mwanadamu mbali na madhara ya Shetani, mbali na majaribio ya Shetani, mbali na ushawishi wa Shetani na kumruhusu mwanadamu aone wazi asili mbovu ya Shetani na uso wake unaotisha. Je, upendo na wasiwasi wa Mungu kwa binadamu ni wa kweli? Ni kitu ambacho kila mmoja wenu anaweza kupitia? (Ndiyo.)

Kumbuka maisha yenu hadi sasa kwa yote ambayo Mungu amekufanyia katika miaka yote ya imani yako. Iwapo unaihisi kwa kina au la, haikuwa ya umuhimu sana? Haikuwa kile ulichohitaji zaidi kupata? (Ndiyo.) Huu si ukweli? Huu si uhai? (Ndiyo.) Je, Mungu amewahi kukupa nuru, na kisha akuulize umpe Yeye chochote kama malipo ya yale yote Aliyokupa wewe? (La.) Kwa hivyo madhumuni ya Mungu ni yapi? Mbona Mungu anafanya hivi? Mungu pia ana lengo la kukumiliki? (La.) Je, Mungu anataka kuwa mfalme katika moyo wa mwanadamu? (Ndiyo.) Kwa hivyo ni nini tofauti kati ya Mungu kuwa mfalme na umiliki wa nguvu wa Shetani? Mungu anataka kupata moyo wa wanadamu, Anataka kumiliki moyo wa mwanadamu—hii inamaanisha nini? Je, inamaanisha kwamba Mungu anataka mwanadamu kuwa vikaragosi Vyake? Mashine Yake? (La.) Kwa hivyo madhumuni ya Mungu ni nini? Kuna tofauti kati ya Mungu kutaka kumiliki moyo wa mwanadamu na umiliki wa nguvu wa Shetani na utawala wa mwanadamu? (Ndiyo.) Tofauti ni nini? Mnaweza kuniambia waziwazi? (Shetani anafanya hivyo kwa nguvu ilhali Mungu anamwacha mwanadamu ajitolee). Je, hii ndiyo tofauti? Mungu anautaka moyo wako Afanyie nini? Na zaidi ya hayo, kwa nini Mungu anataka kukumiliki? Mnaelewa vipi ndani ya mioyo yenu “Mungu anamiliki moyo wa mwanadamu”? Ni lazima tuwe na haki kwa Mungu hapa, vinginevyo watu daima hawataelewa, na kufikiri: “Mungu daima anataka kunimiliki. Anataka kunimiliki kwa nini? Sitaki kumilikiwa, nataka tu kuwa mimi mwenyewe. Mnasema Shetani anawamiliki watu, lakini Mungu pia anawamiliki watu: Haya si sawa? Sitaki kumwacha yeyote kunimiliki. Mimi ni mimi mwenyewe!” Tofauti hapa ni nini? Chukua dakika kuifikiria. Nawauliza, je “Mungu humiliki mwanadamu” ni kirai tupu? Umiliki wa Mungu wa mwanadamu unamaanisha kwamba Anaishi katika moyo wako na anatawala kila neno na kusonga kwako? Akikwambia uketi, huthubutu kusimama? Akikwambia uende Mashariki, huthubutu kwenda Magharibi? Je, ni umiliki unaomaanisha kiti kama hiki? (La, siyo. Mungu anamtaka mwanadamu kuishi kwa kudhihirisha kile Mungu anacho na alicho.) Kwa miaka hii yote Mungu amemsimamia mwanadamu, kwa kazi Yake kwa mwanadamu hadi sasa kwa hatua hii ya mwisho, ni athari ipi imekusudiwa kwa mwanadamu kuhusu maneno yote ambayo Amesema? Je, ni kwamba mwanadamu anaishi kulingana na kile anacho Mungu na alicho? Kwa kuangalia maana halisi ya “Mungu humiliki moyo wa mwanadamu,” inaonekana kama Mungu anachukua moyo wa mwanadamu na kuumiliki, Anaishi ndani yake na Hatoki nje

tena; Anakuwa bwana wa moyo wa mwanadamu na anaweza kutawala na kupanga moyo wa mwanadamu atakavyo, ili mwanadamu lazima atende asemayo Mungu atende. Hali ikiwa hivi, ingeonekana kana kwamba kila mtu anaweza kuwa Mungu na awe na kiini na tabia Yake. Kwa hivyo hapa, mwanadamu pia angeweza kufanya matendo ya Mungu? Je, “umiliki” unaweza kuelezewa kwa njia hii? (La.) Kwa hivyo ni nini? Nawauliza hili: Je, maneno na ukweli wote Mungu anampa mwanadamu ni ufunuo wa kiini cha Mungu na kile Anacho na alichu? (Ndiyo.) Hii ni ya uhakika. Lakini je, maneno yote Mungu anampa mwanadamu ni ya Mungu Mwenyewe kuweka katika vitendo, ya Mungu Mwenyewe kumiliki? Chukua dakika moja kuifikiria? Wakati Mungu anamhukumu mwanadamu, Anafanya hivi kwa sababu ya nini? Maneno haya yalitoka wapi? Ni nini yaliyomo katika maneno haya ambayo Mungu anazungumza Anapomhukumu mwanadamu? Ni nini msingi wake? Msingi wake ni tabia potovu ya mwanadamu? (Ndiyo.) Kwa hivyo athari iliyofikiwa na hukumu ya Mungu ya mwanadamu imetokana na kiini cha Mungu? (Ndiyo.) Kwa hivyo umiliki wa Mungu wa mwanadamu ni kirai tupu? Kwa hakika sicho. Kwa hivyo mbona Mungu anasema maneno haya kwa mwanadamu? Ni nini madhumuni Yake ya kusema maneno haya? Anataka kutumia maneno haya kutumika kama maisha ya mwanadamu? (Ndiyo.) Mungu anataka kutumia ukweli wote huu ambao amezungumza katika maneno haya kutumika kama maisha ya mwanadamu. Wakati mwanadamu anauchukua ukweli huu wote na neno la Mungu na kuyabadilisha katika maisha yake, mwanadamu basi anaweza kumtii Mungu? Mwanadamu basi anaweza kumcha Mungu? Mwanadamu basi anaweza kuepuka maovu? Wakati mwanadamu amefika hapa, anaweza basi kutii ukuu na mipango ya Mungu? Mwanadamu sasa yuko katika nafasi ya kutii mamlaka ya Mungu? Wakati watu kama Ayubu, ama kama Petro wanafika mwisho wa barabara yao, wakati maisha yao yanaweza kufikiwa kuwa yamekomaa, wakati wako na uelewa halisi wa Mungu—Shetani bado anaweza kuwapoteza? Shetani bado anaweza kuwamiliki? Shetani bado anaweza kuwatawala kwa nguvu? (La.) Kwa hivyo huyu ni mtu wa aina gani? Huyu ni mtu ambaye amepatwa kabisa na Mungu? (Ndiyo.) Katika kiwango hiki cha maana, unamwonaje mtu huyu ambaye amepatwa kabisa na Mungu? Kwa Mungu, katika hali hii tayari Amemiliki moyo wa mtu huyu. Lakini mtu huyu anahisi nini? Je, ni kwamba neno la Mungu, mamlaka ya Mungu, na njia ya Mungu yamekuwa uhai ndani ya mwanadamu, basi uhai huu unamiliki utu wote wa mwanadamu, na unafanya yote anayozidi pamoja na kiini chake kutosha kumridhisha Mungu? Kwa Mungu, moyo wa binadamu wakati huu umemilikiwa na Yeye? (Ndiyo.) Mnaelewaje kiwango hiki cha maana sasa? Je, ni Roho wa Mungu anayekumiliki? (La, ni neno la Mungu ambalo linatumiliki.) Ni njia ya Mungu na neno la Mungu ambalo limekuwa maisha yako, na ni ukweli ambao umekuwa maisha yako. Wakati huu, mwanadamu basi ana maisha yanayotoka kwa Mungu, lakini hatuwezi kusema kwamba haya maisha ni maisha ya Mungu. Kwa maneno mengine, hatuwezi kusema kwamba maisha ambayo mwanadamu anapaswa kupata kutoka kwa neno la Mungu ni maisha ya Mungu. Hivyo, licha ya

muda ambao mwanadamu anamfuata Mungu, licha ya idadi ya maneno ambayo mwanadamu anapata kutoka kwa Mungu, mwanadamu hawezi kuwa Mungu. Hata kama siku moja Mungu aseme, “Nimemiliki moyo wako, sasa unamiliki maisha Yangu,” utahisi basi kwamba wewe ni Mungu? (La.) Utakuwa nini basi? Hutakuwa na utii kabisa wa Mungu? Moyo wako hautajawa na maisha ambayo Mungu amekupa? Huu utakuwa udhihirisho wa kawaida kabisa wa kile kinachofanyika wakati Mungu anamiliki moyo wa mwanadamu. Huu ni ukweli. Kwa hivyo kuuangalia kutoka kipengele hiki, mwanadamu anaweza kuwa Mungu? Wakati mwanadamu amepata maneno yote ya Mungu, wakati mwanadamu anaweza kumcha Mungu na kuepukana na maovu, mwanadamu basi anaweza kumiliki utambulisho wa Mungu na kiini cha Mungu? (La.) Licha ya kile kitachofanyika, mwanadamu bado ni mwanadamu wakati yote yamesemwa na kufanywa. Wewe ni kiumbe; wakati umepokea neno la Mungu kutoka kwa Mungu na kupokea njia ya Mungu, unamiliki tu maisha ambayo yanatoka kwa neno la Mungu, na kamwe huwezi kuwa Mungu.

Tukirudia mada yetu hivi sasa, Niliwauliza swali—je, Ibrahimu ni mtakatifu? (La.) Ayubu ni mtakatifu? (La.) Ndani ya utakatifu huu kuna kiini cha Mungu. Mwanadamu hana kiini cha Mungu ama tabia ya Mungu. Hata wakati mwanadamu amepitia maneno yote ya Mungu na amejitayarisha na uhalisi wake, mwanadamu bado hawezi kamwe kuwa na kiini kitakatifu cha Mungu; mwanadamu ni mwanadamu. Mnaelewa, sivyo? Kwa hivyo mnakielewaje kirai hiki “Mungu anakaa katika moyo ya mwanadamu” sasa? (Ni maneno ya Mungu, njia ya Mungu na ukweli Wake yanayokuwa maisha ya mwanadamu.) Umekariri maneno haya. Natumai mtakuwa na uelewa wa kina. Watu wengine wanaweza kuuliza, “Kwa hivyo mbona useme kwamba wajumbe na malaika wa Mungu si watakatifu?” Mnafikiria nini kuhusu swali hili? Labda hamjalifikiria mbeleni. Nitatumia mfano rahisi: Unapowasha roboti, inaweza kucheza ngoma na kuongea, na unaweza kuelewa inachosema. Unaweza kuiita nzuri na yenye uhai, lakini haitaelewa kwa sababu haina uhai. Unapozima uletaji wake wa umeme, bado inaweza kusongasonga? Wakati roboti hii inaamshwa, unaweza kuona ina uhai na ni nzuri. Unaitathmini, iwe ya kina au ya juujuu, lakini iwe vipi macho, unaweza kuiona ikisonga. Lakini unapozima uletaji wake wa umeme, unaona tabia ya aina yoyote kwake? Unaona ikiwa na kiini cha aina yoyote? Unaelewa maana ya kile ninachosema? Hivyo ni kusema, ingawaje roboti hii inaweza kusonga na inaweza kuacha, kamwe hungeweza kuielezea kama kuwa na aina yoyote ya kiini. Huu si ukweli? Hatutazungumzia haya zaidi. Yametosha kwenu kuwa na uelewa wa jumla wa maana. Hebu tutamatishe ushirika wetu hapa. Kwaheri!

Desemba 17, 2013

Tanbihi:

a. “laana inayofungwa na ukanda” ni laana inayotumiwa na mtawa Tang Sanzang katika riwaya ya Kichina Safari ya Magharibi. Anatumia laana hii kumdhiti Sun Wukong kwa kufunga ukanda wa chuma kwenye kichwa cha Sun Wukong, ukimfanya aumwe na kichwa sana, na hivyo kumfanya aweze kudhibitiwa. Imekuwa istiaari ya kueleza kitu kinachomfunga mtu.

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee V

Utakatifu wa Mungu (II)

Leo, kaka na dada, hebu tuimbe wimbo. Tafuta mmoja ambao mnapenda na ambao mmeimba mara nyingi kabla. (Tungependa kuimba wimbo wa neno la Mungu “Upendo Safi Bila dosari.”)

1. “Upendo” unarejelea hisia ambayo ni safi na bila dosari, ambapo mnatumia mioyo yenu kupenda, kuhisi, na kuwa wa kufikiri. Katika upendo hakuna masharti, hakuna vizuizi, na hakuna umbali. Katika upendo hakuna tuhuma, hakuna udanganyifu, na hakuna ujanja. Katika upendo hakuna mabadilishano na hakuna chochote kichafu. Iwapo una upendo, basi hautadanganya, kulalamika, kusali, kuasi, kushurutisha, au kutafuta kupata kitu au kupata kiasi fulani.

2. “Upendo” unarejelea hisia ambayo ni safi na bila dosari, ambapo mnatumia mioyo yenu kupenda, kuhisi, na kuwa wa kufikiri. Katika upendo hakuna masharti, hakuna vizuizi, na hakuna umbali. Katika upendo hakuna tuhuma, hakuna udanganyifu, na hakuna ujanja. Katika upendo hakuna umbali na hakuna chochote kichafu. Iwapo una upendo, basi utajitolea na kuvumilia magumu kwa furaha, na utalingana na Mimi, utaacha kila kitu ulicho nacho kwaajili Yangu, utaacha vyote ulivyo navyo kwa sababu ya Mungu: familia zako, siku zako za baadaye, ujana wako, na ndoa yako. Vinginevyo, upendo wenu haungekuwa upendo hata kidogo, lakini badala yake udanganyifu na usali!

Huu ulikuwa wimbo mzuri kuchagua. Mnapenda kuimba wimbo huu? (Ndiyo.) Mnahisi nini baada ya kuimba wimbo huu? Mnaweza kuhisi upendo wa aina hii ndani yenu? (Bado.) Ni maneno yapi ya wimbo huu yanayokugusa kwa kina zaidi? (Katika upendo hakuna masharti, hakuna vizuizi, na hakuna umbali. Katika upendo hakuna tuhuma, hakuna udanganyifu, hakuna mabadilishano, na hakuna ujanja. Katika upendo hakuna uchaguzi na hakuna chochote kichafu. Lakini ndani yangu bado naona uchafu mwingi, na sehemu zangu nyingi ambazo hujaribu kufanya biashara na Mungu. Kwa kweli sijafikia aina ya upendo ulio safi na usiokuwa na dosari.) Ikiwa hujafikia upendo safi, usio na dosari, basi kiwango cha upendo wako ni kipi? (Niko tu katika hatua ambapo niko tayari kutafuta na nina hamu.) Kulingana na kimo chako mwenyewe na kutumia maneno yako mwenyewe kutoka kwa uzoefu wako mwenyewe, umefikia kiwango kipi? Je, una udanganyifu, una malalamiko? (Ndiyo.) Je, una madai ndani ya moyo wako? Kuna vitu unavyotaka na kutamani kutoka kwa Mungu? (Ndiyo, kuna hivi vitu vilivyo na doa.) Vinajitokeza katika hali gani? (Wakati hali ambayo Mungu amenipangia hailingani na

fikiria zangu ya vile inapaswa kuwa, ama wakati matakwa yangu hayajatimizwa: katika nyakati kama hizi, Ninafunua aina hii ya tabia potovu.) Ninyi ndugu mnaotoka Taiwani, je, ninyi huimba wimbo huu mara kwa mara pia? Je, mnaweza kuzungumza kidogo juu ya jinsi mnavyoelewa “upendo safi bila dosari”? Kwa nini Mungu anafafanua upendo kwa njia hii? (Ninaupenda wimbo huu sana kwa sababu ninaweza kuona kutoka kwao kwamba upendo huu ni upendo kamili. Hata hivyo, bado nina mwendo mrefu kabisa wa kufikia kiwango hicho, na bado niko mbali sana kufikia upendo wa kweli. Kuna vitu ambavyo kwavyo nimeweza kupiga hatua na kushirikiana kupitia nguvu ambayo maneno Yake hunipa na kwa njia ya maombi. Hata hivyo, ninapokabiliwa na majaribu au ufichuzi fulani, mimi huhisi kwamba sina mustakabali au majaliwa, kwamba sina hatima. Wakati kama huo, mimi huhisi dhaifu sana, na suala hili hunisumbua mara nyingi.) Je, ni nini unachozungumzia hasa unaposema “mustakabali na majaliwa”? Je, kuna kitu maalum unachorejelea? Je, ni picha au kitu ulichodhania, au mustakabali na hatima yako ni vitu unavyoweza kuona kweli? Je, ni kitu halisi? Nataka kila mmoja wenu afikirie juu ya jambo hilo: Je, wasiwasi mlio nao kuhusu mustakabali na majaliwa yenu yanarejelea nini? (Ni kuweza kuokolewa ili niweze kuishi.) Ninyi ndugu wengine, ninyi pia huzungumza kidogo juu ya ufahamu wenu wa “upendo safi bila dosari.” (Mtu anapokuwa nao, hakuna uchafu unaotokana na nafsi yake mwenyewe na hadhibitiwi na mustakabali wake au majaliwa yake. Licha ya vile Mungu anamtunza, anaweza kutii kikamilifu kazi ya Mungu na mipango Yake na kumfuata Yeye hadi mwisho kabisa. Upendo wa aina hii tu kwa Mungu ndio upendo safi na usio na dosari. Katika kujipima dhidi yake, nimegundua kwamba, ingawa ninaonekana kuwa nilijitumia au kutupa kando vitu kadhaa katika miaka michache iliyopita ya kumwamini Mungu, sijaweza kweli kumpa Yeye moyo wangu. Wakati Mungu ananifunua, nahisi kwamba siwezi kuokolewa, na nasalia katika hali hasi. Najiona nikifanya wajibu wangu, lakini wakati huo huo najaribu kufanya mipango na Mungu, siwezi kumpenda Mungu kwa moyo wangu wote, na hatima yangu, siku zangu za baadaye, na kudura yangu yote daima yako kwa akili yangu.

Inaonekana kwamba mmepata ufahamu kiasi wa wimbo huu, na mmefanya uhusiano fulani kati ya wimbo huo na matukio yenu halisi. Hata hivyo, mna viwango tofauti vya kukubali kila kirai katika wimbo “Upendo Safi bila Dosari.” Watu wengine hufikiri kwamba ni kutoyaka, watu wengine wanatafuta kuweka kando siku zao za baadaye, watu wengine wanatafuta kuweka kando familia zao, watu wengine hawatafuti kupokea chochote. Bado wengine wanajihitaji kuwa bila udanganyifu, bila malalamiko, na kutoasi dhidi ya Mungu. Kwa nini Mungu angetaka kupendekeza aina hii ya upendo na kuhitaji kwamba watu wampende namna hii? Hii ni aina ya upendo ambao watu wanaweza kuufikia? Hiyo ni kusema, watu wanaweza kupenda namna hii? Watu wanaweza kuona kwamba hawawezi, kwa sababu hawamiliki kamwe upendo wa aina hii.

Wakati hawaumiliki, na kimsingi hawajui kuhusu upendo, Mungu anazungumza maneno haya, ambayo ni mageni kwao. Kwa sababu watu wanaishi katika dunia hii, wanaishi katika tabia yao potovu, iwapo watu wangukuwa na aina hii ya upendo ama iwapo mtu angeweza kumiliki aina hii ya upendo, bila kuwa na maombi na madai, kuwa radhi kujitoa wenyewe na kuwa radhi kustahimili mateso na kuacha vyote vilivyo vyao, mtu anayemiliki aina hii ya upendo angeweza kuonekana katika macho ya watu wengine? Si angekuwa mtu kamili? (Ndiyo.) Mtu kamili kama huyo yupo katika dunia hii? Hayupo, yupo? Mtu wa aina hii hayupo kabisa katika dunia hii, ila angeweza kuishi katika utupu, siyo? Hivyo, watu wengine—kupitia uzoefu wao—wanatumia juhudi nyingi kuwa kama kile ambacho maneno haya yalielezea. Wanajishughulikia, wanajizuia, na hata daima wanajitupa: Wanastahimili mateso na wanaacha dhana ambazo si sahihi walizokuwa nazo. Wanaacha njia walivyokuwa wakiasi Mungu, wanaacha tamaa zao na matakwa. Lakini mwishowe bado hawawezi kufikia mahitaji hayo. Kwa nini hayo yanafanyika? Mungu anasema mambo haya ili kupeana kiwango cha watu kufuata, ili watu wajue kiwango wanachodaiwa na Mungu. Lakini Mungu huwahi kusema kwamba watu lazima wafikie hiki mara moja? Je, Mungu huwahi kusema ni katika wakati upi watu wanapaswa kufikia hiki? (La.) Je, Mungu huwahi kusema kwamba watu lazima wampende namna hii? Kifungu hiki kinasema hivi? La, hakisemi hivi. Mungu anawaambia watu tu kuhusu “upendo” Aliokuwa akirejelea. Kuhusiana na watu kuweza kumpenda Mungu namna hii na kumtendea Mungu namna hii, mahitaji ya Mungu ni yapi? Si muhimu kuyafikia mara moja, ama papo hapo kwa sababu watu hawawezi kufanya hivyo. Mmewahi kufikiria kuhusu masharti ambayo watu wanapaswa kutimiza ili kupenda namna hii? Iwapo watu wangeyasoma maneno haya mara nyingi watakuwa na upendo huu polepole? (La.) Masharti ni yapi basi? Kwanza, watu wanawezaje kuwa huru kutokana na tuhuma kumhusu Mungu? (Ni watu waaminifu tu wanaoweza kufikia jambo hilo.) Je, kuwa huru kutokana na udanganyifu? (Pia wanapaswa kuwa watu waaminifu.) Kuwa mmoja asiyetaka kufanya mipango na Mungu? Huyo pia lazima awe mtu mwaminifu, Je, kutokuwa na ujanja? Kunarejelea nini kusema hakuna chaguo katika upendo? Yote yanarejelea kuwa mtu mwaminifu? Kuna maelezo mengi hapo; uwezo wa Mungu kutaja upendo wa aina hii ama uwezo wa Mungu kufafanua aina hii ya upendo, kusema namna hii, hii inathibitisha nini? Tunaweza kusema kwamba Mungu anamiliki upendo wa aina hii? (Ndiyo.) Mnaona hii wapi? (Kwa upendo Mungu alio nao kwa mwanadamu.) Upendo wa Mungu kwa mwanadamu una sharti? (La.) Kuna vizuizi ama umbali kati ya Mungu na mwanadamu? (La.) Mungu ana tuhuma kumhusu mwanadamu? (La.) Mungu humwangalia mwanadamu na kumwelewa mwanadamu; kwa kweli Anamwelewa mwanadamu. Je, Mungu ni mdanganyifu kwa mwanadamu? (La.) Kwa sababu Mungu anaongea kikamilifu kuhusu upendo huu, moyo Wake ama kiini Chake kinaweza kuwa kamili sana? (Ndiyo.) Watu wamewahi kufafanua upendo kwa njia hii? Mwanadamu amefafanua upendo katika hali gani? Mwanadamu anazungumza vipi kuhusu upendo? Si ni kupeana ama

kutoa? (Ndiyo.) Ufafanuzi wa mwanadamu wa upendo ni rahisi, na hauna kiini.

Ufafanuzi wa Mungu wa upendo na namna Mungu anazungumza kuhusu upendo inahusiana na kipengele cha kiini Chake, lakini kipengele kipi cha kiini Chake? Wakati uliopita tulishiriki kuhusu mada muhimu sana, ni mada ambayo watu wamezungumzia mara nyingi awali, na ni neno ambalo linatajwa mara nyingi katika kipindi cha kumwamini Mungu, lakini ni neno linalojulikana na pia ni geni kwa watu. Lakini mbona hivyo? Ni neno linalotoka kwa lugha za mwanadamu; hata hivyo, miongoni mwa mwanadamu ufafanuzi wake ni dhahiri na pia ni usio dhahiri. Neno hili ni nini? (Utakatifu.) Utakatifu: hiyo ndiyo ilikuwa mada ya wakati wa mwisho tuliposhiriki. Tulishiriki kiasi kuhusu mada hii. Kupitia katika ushirika wetu wa wakati uliopita, je, kila mtu alipata ufahamu mpya kuhusu kiini cha utakatifu wa Mungu? Mnafikiri uelewa mpya ulikuwa nini? Yaani, nini katika uelewa huo ama maneno hayo yaliwafanya kuhisi kwamba uelewa wenu wa utakatifu wa Mungu ulikuwa tofauti ama uliobadilishwa na kile Nilichoshiriki kuhusu utakatifu wa Mungu? Je, uliacha maono? (Mungu anasema Anachohisi katika moyo Wake; ni safi. Hiki ni kipengele kimoja cha utakatifu.) (Kuna utakatifu wakati Mungu ana ghadhabu kwa mwanadamu, hakuna dosari.) (Kuhusu utakatifu wa Mungu, naelewa kwamba kuna ghadhabu ya Mungu na huruma ya Mungu katika tabia Yake ya haki. Hili liliacha mtazamo wenye nguvu kwangu. Katika ushirika wetu wa wakati uliopita, ilitajwa pia kuwa tabia ya Mungu yenye haki ni ya kipekee—sikuelewa jambo hili zamani. Ni baada tu ya kusikia kile ambacho Mungu alikuwa ameshiriki ndipo nilielewa kuwa ghadhabu ya Mungu ni tofauti na hasira ya mwanadamu. Ghadhabu ya Mungu ni kitu chanya na ina maadili; hiyo hutumwa kwa sababu ya kiini cha asili cha Mungu. Mungu huona kitu kibaya, na hivyo Anaachilia ghadhabu Yake. Hiki ni kitu kisicho na kiumbe yeyote aliyeumbwa.) Mada yetu leo ni utakatifu wa Mungu. Watu wote wamesikia na kujifunza kitu kuhusu tabia ya haki ya Mungu. Aidha, watu wengi mara nyingi huzungumza juu ya utakatifu wa Mungu na tabia ya Mungu yenye haki kwa pamoja; wao husema kuwa tabia ya Mungu yenye haki ni takatifu. Neno “takatifu” hakika si geni kwa mtu yeyote—ni neno linalotumiwa mara nyingi. Lakini kwa kuzingatia maana zilizo ndani ya neno hilo, ni maonyesho gani ya utakatifu wa Mungu ambayo watu wanaweza kuona? Ni nini Mungu amefichua ambacho watu wanaweza kutambua? Ninahofia kwamba hiki ni kitu ambacho hakuna anayejua. Tabia ya Mungu ni ya haki, lakini basi ukichukua tabia ya haki ya Mungu na useme kuwa ni takatifu, hiyo inaonekana isiyo dhahiri kiasi, ya kuchanganya wazo; mbona hivi? Unasema tabia ya Mungu ni ya haki, ama unasema tabia Yake ya haki ni takatifu, hivyo katika mioyo yenu mnauainisha utakatifu wa Mungu vipi? Mnauelewa vipi? Hivyo ni kusema, ni nini kuhusu kile ambacho Mungu amefichua, ama kile Anacho na alichuambacho watu wanaweza kutambua kama kitakatifu? Umefikiria hili hapo awali? Kile Nilichoona ni kwamba watu mara nyingi husema maneno yanayotumika sana ama wana virai ambavyo vimesemwa mara kwa

mara, lakini hawajui wanachosema. Hivi tu ni vile kila mtu anavyosema, na wanasema hivi mara nyingi, hivyo inakuwa kirai kilichowekwa. Hata hivyo, iwapo wangechunguza na kutafiti kwa kina maelezo, wangepata kwamba hawajui maana halisi ni nini ama inachorejelea. Kama tu neno “takatifu,” hakuna anayejua kabisa ni kipengele kipi cha kiini cha Mungu kinarejelewa kuhusiana na utakatifu Wake ambao wanaongea kuhusu, na hakuna anayejua kupatanisha neno “takatifu” na Mungu. Watu wamechanganyikiwa mioyoni mwao, na utambuzi wao wa utakatifu wa Mungu ni usio dhahiri na wazi. Kuhusu jinsi Mungu ni mtakatifu hakuna aliye wazi kabisa. Leo tutashiriki kuhusu mada kupatanisha neno “takatifu” na Mungu ili watu waweze kuona maudhui ya kweli ya kiini cha utakatifu wa Mungu, na hili litazuia watu wengine kulitumia neno hilo kimazoea ovyo ovyo na kusema vitu kwa nasibu wakati hawajui maana yake, ama kama wako sawa na sahihi. Watu daima wamekuwa wakizungumza namna hii; wewe umefanya, yeye pia na hivyo imekuwa tabia ya usemi. Bila kukusudia inaharibu neno kama hilo.

Kuhusu neno “takatifu,” juujuu linaonekana rahisi sana kuelewa, siyo? Kwa kiwango cha chini kabisa watu wanaamini neno “takatifu” linamaanisha nadhifu, isiyo na doa, tukufu, na safi. Kuna watu wengine pia ambao huhusisha “takatifu” na “upendo,” ambayo ni sahihi; hii ni sehemu yake. Upendo wa Mungu ni sehemu ya kiini Chake, lakini si kiini chote. Hata hivyo, katika mitazamo ya watu, wanaona neno na kulishirikisha na vitu ambavyo wao wenyewe wanaviona kuwa nadhifu na safi, ama na vitu ambavyo wao binafsi wanafikiri havina doa wala havina dosari. Kwa mfano, watu wengine walisema kwamba ua la yungiyungi ni safi, na kwamba linatoa maua bila dosari kutoka kwa maji machafu. Hivyo watu wakaanza kutumia neno “takatifu” kwa ua la yungiyungi. Watu wengine walichukulia hadithi za mapenzi zilizobuniwa na wengine kuwa takatifu, ama wangemchukulia mhusika mkuu anayestahili upaa kuwa mtakatifu. Zaidi, wengine walifikiria watu kutoka kwa Biblia, ama wengine walioandikwa katika vitabu vya kiroho—kama watakatifu, mitume, au wengine ambao walimfuata Mungu awali Alipokuwa akifanya kazi Yake—kama waliokuwa na uzoefu wa kiroho ambao ulikuwa takatifu. Haya yote ni mambo yaliyofikiriwa na watu na hizi ni dhana zinazoshikiliwa na watu. Mbona watu wanashikilia dhana kama hizi? Sababu ni rahisi sana: Ni kwa sababu watu wanaishi miongoni mwa tabia potovu na wanaishi katika dunia ya uovu na uchafu. Kila kitu wanachooona, kila kitu wanachogusa, kila kitu wanachopitia ni uovu wa Shetani na upotovu wa Shetani na pia kufanya mipango, kupigana wenyewe kwa wenyewe, na vita vinavyotokea miongoni mwa watu walio chini ya ushawishi wa Shetani. Kwa hivyo, hata wakati Mungu anafanya kazi Yake kwa watu, na hata wakati Anazungumza nao na kufichua tabia na kiini Chake hawawezi kuona ama kujua utakatifu na kiini cha Mungu ni nini. Watu mara nyingi husema kwamba Mungu ni mtakatifu, lakini hawana uelewa wowote wa kweli; wao husema tu maneno matupu. Kwa sababu watu wanaishi miongoni mwa uchafu na upotovu na wanamilikiwa na Shetani, na hawaoni mwangaza,

hawajui chochote kuhusu masuala mema na zaidi, hawajui ukweli. Kwa hivyo, hakuna anayejua maana ya takatifu. Baada ya kusema hayo, kuna vitu vitakatifu ama watu watakatifu miongoni mwa binadamu hawa potovu? Tunaweza kusema kwa uhakika La, hakuna, kwa sababu kiini cha Mungu tu ndicho kitakatifu.

Kuhusu utakatifu wa kiini cha Mungu, wakati uliopita tulishiriki kidogo kuuhusu na huo ulikuwa msukumo wa maarifa ya watu ya utakatifu wa Mungu, lakini hautoshi. Hauwezi kutosha kusaidia watu kujua kikamilifu utakatifu wa Mungu, wala hautoshi kuwasaidia kuelewa kwamba utakatifu wa Mungu ni wa kipekee. Zaidi, hautoshi kuruhusu watu kuelewa kipengele cha maana ya ukweli ya utakatifu kwani imejumuishwa kabisa kwa Mungu. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba tuendeleo na ushirika wetu katika mada hii. Hapo nyuma ushirika wetu ulijadili mada tatu, kwa hivyo sasa tunapaswa kujadili mada ya nne, na tutaanza kusoma maandiko.

Majaribu ya Shetani

Mat 4:1-4 Baada ya hapo Yesu akaongozwa mwituni na Roho kwa minajili ya kujaribiwa na ibilisi. Na baada ya Yeye kufunga kwa siku arobaini mchana na usiku, Alihisi njaa. Na aliyemjaribu alipokuja Kwake, alimwambia, Iwapo Wewe ni Mwana wa Mungu, yaamrishe mawe haya yabadilike mikate. Lakini Akamjibu na kusema, imeandikwa, Mwanadamu hatadumu kwa mkate pekee, lakini kwa kila neno linalotoka kinywani mwa Mungu.

Haya ndiyo maneno ambayo ibilisi kwanza alijaribu kumjaribu Bwana Yesu. Ni nini maudhui ya aliyoyasema ibilisi? (“Iwapo Wewe ni Mwana wa Mungu, yaamrishe mawe haya yabadilike mikate.”) Maneno haya ambayo ibilisi alizungumza ni rahisi kiasi, lakini kuna tatizo na kiini chake? Ibilisi alisema, “Iwapo Wewe ni Mwana wa Mungu,” lakini katika moyo wake, alijua au hakujua kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu? Alijua au hakujua kwamba Alikuwa Kristo? (Alijua.) Basi kwa nini alisema “Iwapo Wewe ni”? (Alikuwa akijaribu kumjaribu Mungu.) Lakini ni nini madhumuni ya kufanya hivyo? Alisema, “Iwapo Wewe ni Mwana wa Mungu.” Katika moyo wake alijua kwamba Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu, alijua haya vizuri sana moyoni mwake, lakini licha ya kujua haya, je, alinyenyekea Kwake na kumwabudu Yeye? (La.) Alitaka kufanya nini? Alitaka kutumia mbinu hii na maneno haya kumghadhabisha Bwana Yesu, na kisha kumhadaa Atende kulingana na makusudi yake. Je, si hii ndiyo iliyokuwa maana ya maneno ya ibilisi? Katika moyo wa Shetani, alijua wazi kwamba huyu alikuwa Bwana Yesu Kristo, lakini alisema maneno haya hata hivyo. Je, si hii ni asili ya Shetani? Asili ya Shetani ni nini? (Kuwa mjanja, mwovu na kutokuwa na Heshima kwa Mungu.) Ni matokeo gani yangetokana na kutomcha Mungu? Je, si kwamba alitaka kumshambulia Mungu? Alitaka kutumia mbinu hii kumshambulia Mungu, na hivyo alisema: “Iwapo Wewe ni Mwana wa Mungu, yaamrishe mawe haya yabadilike mikate”; je, si hii ni nia ovu ya Shetani?

Alikuwa anajaribu kufanya nini kweli? Lengo lake ni wazi sana: Alikuwa anajaribu kutumia mbinu hii kukanusha nafasi na utambulisho wa Bwana Yesu Kristo. Alichomaanisha na maneno hayo ni, “Iwapo wewe ni Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Usipo, basi wewe siwe Mwana wa Mungu na Hufanyi kazi hii.” Hii ni sahihi? Alitaka kutumia mbinu hii kumshambulia Mungu, alitaka kuvunja na kuharibu kazi ya Mungu; huu ndio uovu wa Shetani. Uovu wake ni maonyesho ya kiasili ya asili yake. Ingawaje alijua Bwana Yesu Kristo alikuwa Mwana wa Mungu, kupata mwili kwenyewe kwa Mungu Mwenyewe, hangeweza kuwacha kufanya kitu kama hiki, kumfuata Mungu nyuma na kuendelea kumshambulia na kujaribu sana kuvuruga na kuharibu kazi ya Mungu.

Sasa, hebu tuchambue kirai hiki alichonena Shetani: “Yaamrishe mawe haya yabadilike mikate” Kubadili mawe yawe mikate—hili linamaanisha chochote? Iwapo kuna chakula, mbona usile? Mbona ni muhimu kubadili mawe yawe mikate? Kuna maana hapa? Ingawa alikuwa amefunga wakati huo, kwa hakika Bwana Yesu alikuwa na chakula cha kula? (Alikuwa nacho.) Kwa hivyo, hapa, tunaona upumbavu wa matumizi ya Shetani ya kirai hiki. Kwa ujanja na uovu wake wote, tunaona upumbavu na upuuzi wake. Shetani anafanya idadi fulani ya mambo. Unaona asili yake yenye kudhuru na unaona akiharibu kazi ya Mungu, na wa kuchukiza na kuudhi sana. Lakini kwa upande mwingine, unapata asili ya kitoto na ujinga nyuma ya maneno na vitendo vyake? Huu ni ufunuo kuhusu asili ya Shetani; ana asili ya aina hii na atafanya kitu kama hiki. Kwa wanadamu, kirai hiki ni cha upuuzi na cha kuchekesha. Lakini maneno kama hayo kwa hakika yanaweza kutamkwa na Shetani. Tunaweza kusema kwamba ni asiyejua? Mjinga? Uovu wa Shetani uko kila mahali na daima unafichuliwa. Na Bwana Yesu anamjibu aje? (“Mwanadamu hatadumu kwa mkate pekee, lakini kwa kila neno linalotoka kinywani mwa Mungu.”) Maneno haya yana nguvu yoyote? (Yanayo.) Mbona tunasema kwamba yana nguvu? Hii ni kwa sababu maneno haya ni ukweli. Sasa, mtu anaishi kwa mkate tu? Bwana Yesu alifunga kwa siku na usiku 40. Alikufa kwa njaa? (La.) Hakufa kwa njaa, kwa hivyo Shetani alimkaribia, akimwambia abadili mawe yawe chakula kwa kusema kitu kama hiki: “Ukiyabadili mawe yawe chakula, Hutakuwa basi na vitu vya kula? Si basi Hutalazimika kufunga, Hutalazimika kuwa na njaa?” Lakini Bwana Yesu alisema, “Mwanadamu hatadumu kwa mkate pekee,” inayomaanisha kwamba, ingawa mwanadamu anaishi katika mwili, kile kinachouruhusu mwili wake kuishi na kupumua si chakula, ila maneno yote yaliyotamkwa na kinywa cha Mungu. Katika upande mmoja, maneno haya ni ukweli; yanawapa watu imani, yakiwafanya wahisi kwamba wanaweza kumtegemea Mungu na kwamba Yeye ni ukweli. Kwa upande mwingine, kuna kipengele cha vitendo katika maneno haya? Si Bwana Yesu bado amesimama pale na bado Yu hai baada ya kufunga kwa siku na usiku 40? Huu si mfano? Hajakula chakula chochote kwa siku na usiku 40. Bado yuko hai. Huu ni ushahidi wa nguvu unaothibitisha ukweli

wa maneno Yake. Maneno haya ni rahisi, lakini kwa Bwana Yesu, je, Aliyazungumza tu wakati ambapo Shetani alimjaribu, au yalikuwa tayari pamoja na Yeye? Kuliweka kwa njia nyingine, Mungu ni ukweli, Mungu ni uhai, lakini je, ukweli na uhai wa Mungu uliongezwa kwa kuchelewa? Ulitokana na uzoefu? La, ni ya asili ndani ya Mungu, Ambayo inamaanisha ukweli na uhai vipo ndani ya kiini cha Mungu. Licha ya kile kinachomfanyikia, Anachofichua ni ukweli. Ukweli huu, kirai hiki—iwapo maudhui yake ni mapana ama finyu—kinaweza kumwacha mwanadamu aishi, kimpote uhai; kinaweza kumwezesha mwanadamu kupata, ndani yake, ukweli, uwazi kuhusu njia ya maisha ya binadamu, na kumwezesha kuwa na imani kwa Mungu. Kwa maneno mengine, ndicho chanzo cha matumizi ya Mungu ya kirai hiki ni chema. Hivyo tunaweza kusema kitu hiki chema ni takatifu? (Ndiyo.) Kirai cha Shetani kinatoka kwa asili ya Shetani. Shetani anafichua asili yake ovu, asili yake yenye kijicho, kila mahali, daima. Sasa, ufunuo huu, Shetani anaufanya kiasili? Kuna yeyote anayemchochea? Kuna yeyote anayemsaidia? Kuna yeyote anayemshurutisha? (La.) Anautoa kwa hiari yake mwenyewe. Hii ni asili ovu ya Shetani. Licha ya kile Mungu anafanya na jinsi Anavyokifanya, Shetani yuko nyuma Yake. Kiini na sura ya ukweli ya vitu hivi ambavyo Shetani anasema na kufanya ni kiini cha Shetani—kiini ovu, kiini cha kuonea kijicho. Sasa, kuendelea kusoma, ni nini tena Shetani anasema? Tuendeleo kusoma hapa chini.

Mat 4:5-7 Kisha Ibilisi akamchukua hadi katika mji mtakatifu, na kumweka juu ya kinara cha hekalu, Naye akamwambia, Ikiwa Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, jirushe chini: kwa kuwa imeandikwa, Atawaamuru malaika Wake wakuchunge: na watakubeba mikononi mwao, usije ukaukwaa mguu wako kwenye jiwe wakati wowote. Yesu akamwambia, Imeandikwa tena, Usimjaribu Bwana Mungu wako.

Hebu kwanza tuone maneno ambayo Shetani alizungumza hapa. Shetani alisema “Ikiwa Wewe ndiwe Mwana wa Mungu, jirushe chini,” na kisha akadondoa kutoka kwa maandiko, “Atawaamuru malaika Wake wakuchunge: na watakubeba mikononi mwao, usije ukaukwaa mguu wako kwenye jiwe wakati wowote.” Unahisi vipi unaposikia maneno ya Shetani? Si ni ya kitoto sana? Ni ya kitoto, upuuzi na kuchukiza. Mbona Nasema hivi? Daima Shetani hufanya kitu kijinga, anaamini kwamba ni mwerevu sana; na mara nyingi hutaja maandiko—hata neno la Mungu—anajaribu kuyabadili maneno haya dhidi ya Mungu kumshambulia na kumjaribu. Lengo lake la kufanya hivi ni kuharibu mpango wa kazi ya Mungu. Je, unaweza kuona chochote katika maneno haya yaliyonenwa na Shetani? (Shetani huwa na nia mbaya) Katika kila ambacho Shetani hufanya, kila mara yeye hutafuta kuwajaribu binadamu. Shetani hazungumzi kwa njia inayoeleweka rahisi, bali kwa njia isiyo wazi akitumia majaribu, ulaghai na ushawishi. Shetani anachukulia kumjaribu kwake Mungu kana kwamba Yeye alikuwa binadamu wa kawaida, akiamini kwamba Mungu pia ni asiyejua, mjinga, na asiyeweza kutofautisha kwa wazi vitu

vilivyo. Shetani anafikiri kwamba Mungu na pia mwanadamu hawataona hadi kwa kiini chake na kwamba Mungu na mwanadamu wote hawataona udanganyifu wake na nia zake mbaya. Si hapa ndipo Shetani anapata ujinga wake? Zaidi, Shetani anataja maandiko wazi; anafikiria kwamba kufanya hivyo kunamfanya kuaminika, na kwamba hutaweza kuona dosari zozote kwa haya ama kuepuka kudanganywa na haya. Si hapa ndipo Shetani anakuwa mjinga na kama mtoto? Hii ni kama wakati watu wengine wanaeneza injili na kuwa na ushuhuda kwa Mungu, si wasioamini watasema kitu kama alichosema Shetani? Mmesikia watu wakisema kitu kama hiki? Ni jinsi gani unahisi kuchukizwa unaposikia vitu kama hivyo? Unahisi kuchukizwa? (Ndiyo.) Unapohisi kuchukizwa, pia unahisi kutiwa kinyaa na kukirihishwa? Unapokuwa na hisia hizi unaweza kutambua kwamba Shetani na tabia potovu ambayo Shetani anamfanyia mwanadamu ni ovu? Katika mioyo yenu mmewahi kuwa na utambuzi kama, “Maneno ya Shetani yanaleta mashambulizi na majaribu, maneno yake ni ya ujinga, ya kuchekeka, ya kitoto, na ya kuchukiza. Hata hivyo, katika matamshi ya Mungu na vitendo vya Mungu, Hangetumia mbinu kama hizi kuzungumza ama kufanya kazi Yake, na Hajawahi kufanya hivyo”? Bila shaka, katika hali hii watu wana tu kiasi kidogo cha kuhisi kuendelea na hawana utambuzi wa utakatifu wa Mungu, sivyo? Na kimo chenu cha sasa, mnahisi tu hivi: “Kila kitu Mungu anasema ni ukweli, ni cha manufaa kwetu, na lazima tukikubali”; bila kujali iwapo unaweza kukubali hili au la, bila ubaguzi unasema kwamba maneno ya Mungu ni ukweli na kwamba Mungu ni ukweli, lakini hujui kwamba ukweli ni utakatifu wenyewe na kwamba Mungu ni mtakatifu.

Hivyo, jibu la Yesu kwa maneno haya ya Shetani lilikuwa lipi? Yesu alimwambia: “Imeandikwa tena, Usimjaribu Bwana Mungu wako.” Kuna ukweli katika maneno haya ambayo Yesu alisema? (Ndiyo.) Kuna ukweli ndani yake. Juujuu inaonekana maneno haya ni amri ya watu kufuata, ni kirai rahisi, lakini hata hivyo, mwanadamu na Shetani wamekiuka maneno haya mara nyingi. Hivyo, Bwana alimwambia Shetani, “Usimjaribu Bwana Mungu wako.” kwa sababu hiki ndicho kile Shetani alifanya mara nyingi na alifanya kila juhudi kufanya hivyo, unaweza hata kusema kwamba Shetani alifanya hivyo bila haya. Ni asili ya msingi ya Shetani kutomcha Mungu na kutomheshimu Mungu kwa moyo wake. Hata wakati Shetani alikuwa kando ya Mungu na angeweza kumwona, Shetani hakuweza kuacha kumjaribu Mungu. Kwa hivyo, Bwana Yesu alimwambia Shetani, “Usimjaribu Bwana Mungu wako.” Hiki ni kirai ambacho Mungu amemwambia Shetani mara nyingi. Si kutumia kirai hiki kuna faa hata leo? (Ndiyo, kwani pia sisi humjaribu Mungu mara nyingi.) Mbona watu hufanya hivyo mara nyingi? Je, ni kwa sababu watu wamejawa na tabia potovu ya kishetani? (Ndiyo.) Kwa hivyo kile Shetani alisema hapa juu ni kitu ambacho watu husema mara nyingi? Na katika hali gani? Mtu anaweza kusema kwamba watu wamekuwa wakisema mambo kama haya licha ya wakati na mahali. Hii inadhihirisha kwamba tabia ya watu ni sawa kabisa na tabia potovu ya Shetani.

Bwana Yesu alisema kirai rahisi, ambacho kinawakilisha ukweli na ambacho watu wanahitaji. Hata hivyo, katika hali hii Bwana Yesu alikuwa akigombana na Shetani? Kulikuwa na chochote cha kukabiliana kwa kile Alisema kwa Shetani? (La.) Bwana Yesu aliyachukulia vipi majaribu ya Shetani kwa moyo Wake? Je, Alihisi kuchukizwa na kutiwa kinyaa? (Ndiyo.) Bwana Yesu alihisi kutiwa kinyaa na kuchukizwa lakini Hakugombana na Shetani, wala hata chini zaidi Hakuzungumza kuhusu kanuni zozote kubwa. Kwa nini hivyo? (Kwa sababu Shetani daima yuko hivyo, hawezi kubadilika.) Tunaweza kusema kwamba Shetani hana akili? (Ndiyo, tunaweza.) Je, Shetani anaweza kutambua kwamba Mungu ni ukweli? Shetani hatawahi kutambua kwamba Mungu ni ukweli na hatawahi kukubali kwamba Mungu ni ukweli; hii ni asili yake. Zaidi, kuna kitu kingine kuhusu asili ya Shetani kinachotia kinyaa, ni nini? Katika majaribio yake ya kumjaribu Bwana Yesu, Shetani alifikiri kwamba, hata kama alimjaribu Mungu na hangefaulu, bado angejaribu jambo hili tu. Hata kama angeadhibiwa, angeifanya tu. Hata kama hangepata chochote chema kutoka kwa kufanya hivyo, angeifanya tu, na kuendelea na kusimama dhidi ya Mungu hadi mwisho kabisa. Hii ni asili ya aina gani? Si huo ni uovu? Yule anayekasirika sana wakati Mungu anatajwa, yule anayekuwa na hasira wakati Mungu anatajwa, amemwona Mungu? Anamjua Mungu? Hajui Mungu ni nani, hamwamini, na Mungu hajaongea naye. Mungu hajawahi kumsumbua, kwa hivyo mbona akuwe na hasira? Tunaweza kusema kwamba mtu huyu ni mwovu? Mitindo ya kidunia, kula, kunywa, na kutafuta raha, na kufuata watu mashuhuri—hakuna chochote kati ya vitu hivi kitakachomsumbua mwanadamu kama huyo. Hata hivyo, “Mungu” akitajwa tu au ukweli wa maneno ya Mungu, yeye anashikwa na hasira ghafla. Je, si huku kunajumuisha kuwa na asili ya uovu? Hili linatosha kuthibitisha kwamba hii ni asili ya uovu ya mwanadamu. Sasa, mkijizungumzia, kuna wakati ambapo ukweli unatajwa, ama wakati majaribio ya Mungu kwa mwanadamu yanatajwa ama wakati maneno ya Mungu ya hukumu dhidi ya mwanadamu yanatajwa, na mnahisi kusumbuliwa, kutiwa kinyaa, na hamtaki kusikia kuyahusu? Mioyo yenu inaweza kufikiri: Si watu wote walisema kwamba Mungu ni ukweli? Baadhi ya maneno haya si ukweli, haya bila shaka ni maneno ya Mungu ya maonyo kwa mwanadamu! Watu wengine hata wanaweza kuhisi kuchukizwa kwa mioyo yao: Haya yanatajwa kila siku, majaribio Yake kwetu daima yanatajwa kama hukumu Yake; haya yote yataisha lini? Tutapokea lini hatima njema? Haijulikani hasira hii isiyo na busara inatoka wapi. Hii ni asili ya aina gani? (Asili ovu.) Inasababishwa na asili ovu ya Shetani. Na kwa Mungu kuhusu asili ovu ya Shetani na tabia potovu ya mwanadamu, Hagombani kamwe wala kubishana na watu, na kamwe Halalamiki wakati watu wanatenda kutokana na ujinga. Hamtamwona Mungu akiwa na mitazamo sawa kuhusu vitu ambavyo watu wanavyo, na zaidi hamtamwona Akitumia maoni ya wanadamu, maarifa yao, sayansi yao ama filosofia yao ama fikira za mwanadamu kushughulikia vitu, Badala yake, kila kitu anachofanya Mungu na kila kitu Anachofichua kinahusiana na ukweli. Yaani, kila neno ambalo amesema na kila kitendo

amefanya kinahusiana na ukweli. Ukweli huu sio tu ndoto isiyo na msingi; ukweli huu na maneno haya yanaelezwa na Mungu kwa sababu ya kiini cha Mungu na uhai Wake. Kwa sababu maneno haya na kiini cha kila kitu Mungu amefanya ni ukweli, tunaweza kusema kwamba kiini cha Mungu ni kitakatifu. Kwa maneno mengine, kila kitu ambacho Mungu anasema na kufanya kinaleta uzima na mwangaza kwa watu, kinawaruhusu watu kuona vitu vizuri na uhalisi wa vitu hivyo vizuri, na kinaashiria wanadamu njia ili watembelee njia njema. Vitu hivi vinaamuliwa kwa sababu ya kiini cha Mungu na vinaamuliwa kwa sababu ya kiini cha utakatifu Wake. Mmekiona, siyo? Tutaendelea kuyasoma maandiko.

Mat 4:8-11 Tena, Ibilisi akampeleka hadi kwenye mlima mrefu sana, na kumwonyesha falme zote za dunia, na fahari yao; Na akamwambia, Hivi vyote nitakupa Wewe, Ukianguka chini na kuniabudu. Kisha Yesu akamwambia, Ondoka uende zako, Shetani; kwa kuwa imeandikwa, Muabudu Bwana Mungu wako, na ni Yeye peke Yake ndiye utakayemtumikia. Basi Akawachwa na Ibilisi, na, tazama, malaika wakaja na wakamhudumia.

Shetani, ibilisi, baada ya kushindwa katika hila zake mbili za awali, alijaribu nyingine tena: Alionyesha falme zote duniani na utukufu wa falme hizi kwa Bwana Yesu na kumwambia amwabudu ibilisi. Unaona nini kuhusu sura za ukweli za ibilisi kutoka kwa hali hii? Si Shetani ibilisi hana haya kabisa? (Ndiyo.) Anaweza kukosa haya namna gani? Kila kitu kiliumbwa na Mungu, lakini Shetani anakigeuza na kumwonyesha Mungu akisema, “Angalia utajiri na utukufu wa falme hizi zote. Hivi vyote nitakupa, ukianguka chini na kuniabudu.” Je, si hili ni mabadiliko ya jukumu? Si Shetani hana haya? Mungu aliumba kila kitu, lakini kilikuwa cha raha Zake? Mungu alimpa mwanadamu kila kitu, lakini Shetani alitaka kunyakua vyote na baadaye akasema, “Niabudu! Niabudu na nitakupa Wewe haya yote.” Huu ni uso usiopendeza wa Shetani; hana haya kabisa! Shetani hata hajui maana ya neno “haya,” na huu ni mfano mwingine tu wa uovu wake. Hata hajui haya ni nini. Shetani anajua vyema kwamba Mungu aliumba kila kitu na kwamba Anavisimamia na Anavitawala. Kila kitu ni cha Mungu, si cha mwanadamu, sembuse Shetani, lakini Shetani ibilisi bila haya alisema kwamba angempa Mungu kila kitu. Si tena Shetani anafanya kitu cha ujinga na kisicho na aibu? Mungu anamchukia Shetani hata zaidi sasa, siyo? Lakini licha ya kile Shetani alijaribu kufanya, Bwana Yesu alikiamini? Bwana Yesu alisema nini? (“Muabudu Bwana Mungu wako na umtumikie Yeye pekee.”) Je, kirai hiki kina maana ya utendaji? (Ndiyo.) Maana gani ya utendaji? Tunaona uovu na kutokuwa na aibu kwa Shetani katika matamshi yake. Kwa hivyo iwapo mwanadamu angemwabudu Shetani, hitimisho lingekuwa nini? Angepokea utajiri na utukufu wa falme zote? (La.) Angepokea nini? Je, wanadamu wangukuwa wasio na haya na wa kuchekwa kama tu Shetani? (Ndiyo.) Hawangukuwa tofauti na Shetani basi. Kwa hivyo, Bwana Yesu alisema maneno haya ambayo ni muhimu kwa kila mwanadamu: “Muabudu Bwana Mungu wako, na ni Yeye peke Yake ndiye

utakayemtumikia,” kinachosema kwamba isipokuwa Bwana, isipokuwa Mungu Mwenyewe, ukimhudumia mwingine, ukimwabudu Shetani ibilisi, basi utagaagaa katika uchafu sawa na Shetani. Kisha utashiriki kutokuwa na haya na uovu wa Shetani, na kama tu Shetani ungemjaribu Mungu na kumshambulia Mungu. Na basi mwisho wako ungekuwa upi? Ungechukiwa na Mungu, kuangushwa na Mungu na kuangamizwa na Mungu. Baada ya Shetani kumjaribu Bwana Mungu mara kadhaa bila mafanikio, alijaribu tena? Shetani hakujaribu tena na kisha akaondoka. Hii inathibitisha nini? Inathibitisha kwamba asili ovu ya Shetani, kuonea kijicho kwake, na ujinga na upuuzi wake yote hayastahili kutajwa mbele ya Mungu. Bwana Yesu alimshinda Shetani kwa sentensi tatu tu, na baadaye akatoroka na mkia wake katikati ya miguu yake, kuaibika sana asiweze kuonyesha uso wake tena, na hakumjaribu Bwana Yesu tena. Kwa sababu Bwana Yesu alikuwa amelishinda jaribio hili la Shetani, Angeweza kuendelea kwa urahisi kazi ambayo Alipaswa kufanya na kuanza kazi zilizokuwa mbele Yake. Je, yote aliyoyasema Bwana Yesu na kufanya katika hali hii yanabeba maana kiasi ya vitendo kwa kila mtu yakitumika sasa? (Ndiyo.) Maana ya utendaji ya aina gani? Je, kumshinda Shetani ni kitu rahisi kufanya? Ni lazima watu wawe na uelewa wazi wa asili ovu ya Shetani? Ni lazima watu wawe na uelewa sahihi wa vishawishi vya Shetani? (Ndiyo.) Unapopitia vishawishi vya Shetani katika maisha yako, na iwapo unaweza kuona hadi kwa asili ovu ya Shetani, utaweza kumshinda? Iwapo unajua kuhusu ujinga na upuuzi wa Shetani, bado unaweza kusimama kando ya Shetani na kumshambulia Mungu? Ikiwa unaelewa jinsi kuwa na kijicho na kutokuwa na aibu kwa Shetani vinafichuliwa kupitia kwako—iwapo unatambua wazi na kujua mambo haya—bado ungemshambulia na kumjaribu Mungu kwa njia hii? (La, hatungeweza.) Utafanya nini? (Tutaasi dhidi ya Shetani na kumwacha.) Hili ni jambo rahisi kufanya? Hili si rahisi, kufanya hivi, watu wanalazimika kuomba mara nyingi, ni lazima wajiweke mbele ya Mungu na wajichunguze. Na lazima waache kufundisha nidhamu kwa Mungu na hukumu Yake na kuadibu Kwake viwajie. Ni kwa njia hii tu ndiyo watu wataweza kujinasua polepole kutoka kwa udanganyifu na udhibiti wa Shetani.

Tunaweza kuweka pamoja mambo yanayojumuisha kiini cha Shetani kutoka kwa mambo haya ambayo amesema. Kwanza, kiini cha Shetani kwa jumla kinaweza kusemwa kuwa ovu, ambacho ni kinyume na utakatifu wa Mungu. Kwa nini Nasema kiini cha Shetani ni ovu? Mtu anapaswa kuangalia matokeo ya kile Shetani anafanyia watu ili kuona haya. Shetani anapotosha na kudhibiti mwanadamu, na mwanadamu anatenda chini ya tabia potovu ya Shetani, na anaishi katika dunia ya watu waliopotoshwa na Shetani. Binadamu wanamilikiwa na kusimilishwa na Shetani bila kujua; mwanadamu hivyo ana tabia potovu ya Shetani, ambayo ni asili ya Shetani. Kutoka kwa yote Shetani amesema na kufanya, umeona kiburi chake? Umeona udanganyifu na kijicho chake? Kiburi cha Shetani kimsingi kinaonekana vipi? Je, Shetani daima anataka

kuchukua nafasi ya Mungu? Shetani daima anataka kuharibu kazi ya Mungu na nafasi ya Mungu na kuyachukua kuwa yake ili watu waunge mkono na kuabudu Shetani; hii ni asili ya kiburi ya Shetani. Wakati Shetani anapotosha watu, huwaambia moja kwa moja kile wanachopaswa kufanya? Wakati Shetani anamjaribu Mungu, je, hatoki na kusema, “Nakujaribu, nitakushambulia”? Hakika hafanyi hivyo. Ni mbinu gani hivyo Shetani anatumia? Anashawishi, anajaribu, anashambulia, na anaweka mitego yake, na hata kwa kutaja maandiko, Shetani anazungumza na kutenda kwa njia mbalimbali ili kutimiza dhamira na nia zake mbaya. Baada ya Shetani kufanya hivi, ni nini kinachoweza kuonekana kutoka kile kilichojitokeza kwa mwanadamu? Je, si watu wana kiburi? Mwanadamu ameteseka kutoka kwa upotovu wa Shetani kwa maelfu ya miaka na hivyo mwanadamu amekuwa mwenye kiburi mdanganyifu, mwenye kijicho, na asiyeifikiri. Haya mambo yote yametokana kwa sababu ya asili ya Shetani. Kwa sababu asili ya Shetani ni ovu, amempa mwanadamu asili hii ovu na kumletea mwanadamu tabia hii potovu. Kwa hivyo, mwanadamu anaishi chini ya tabia potovu ya kishetani na, kama Shetani, mwanadamu anaenda kinyume na Mungu, anamshambulia Mungu, na kumjaribu Yeye hadi kwa kiwango ambacho mwanadamu hamwabudu Mungu na hamheshimu katika moyo wake.

Kuhusu utakatifu wa Mungu, hata kama inaweza kuwa mada inayojulikana, ni mada ambayo, inapozungumziwa, inaweza kuwa dhahania kiasi kwa watu wengine na inaweza inaweza kuwa ya kina na isiyofikiwa. Lakini hakuna haja ya kuwa na wasiwasi. Nitawasaidia kuelewa maana ya utakatifu wa Mungu. Kuelewa mtu fulani ni mtu wa aina gani, angalia kile anachofanya na matokeo ya vitendo vyake, na kisha utaweza kuona kiini cha mtu huyo. Inaweza kusemwa hivyo? (Ndiyo.) Basi, hebu tushiriki kuhusu utakatifu wa Mungu kutoka kwa mtazamo huu kwanza. Kwa maneno mengine kiini cha Shetani ni ovu, na kwa hivyo vitendo vya Shetani kwa mwanadamu vimekuwa kumpotosha bila kikomo. Shetani ni mwovu, kwa hivyo watu ambao amepotosha hakika ni waovu, siyo? Kuna yeyote anayeweza kusema, “Shetani ni mwovu, pengine mtu aliyepotosha ni mtakatifu”? Ni mzaha, siyo? Je, hata inawezekana? (La.) Shetani ni mwovu, na ndani ya uovu wake kuna upande muhimu na pia wa vitendo. Haya si mazungumzo matupu tu. Hatujaribu kusema uwongo juu ya Shetani; tunashiriki tu kuhusu ukweli na uhalisi. Hii inaweza kuumiza watu wengine ama sehemu fulani ya watu, lakini hakuna nia mbaya hapa; pengine mtasikia haya leo na kuhisi kutostareheka kiasi, lakini siku fulani hivi punde, wakati mnaweza kumtambua, mtajichukia, na mtahisi kwamba kile tulichozungumzia leo ni cha manufaa kwenu na chenye thamani. Kiini cha Shetani ni ovu, kwa hivyo matokeo ya vitendo vya Shetani bila shaka ni ovu, ama kwa kiwango cha chini kabisa, yanahusiana na uovu wake, tunaweza kusema hayo? (Ndiyo.) Kwa hivyo, je Shetani anampotosha mwanadamu vipi? Kuhusu uovu anaoufanya Shetani duniani na miongoni mwa binadamu, ni vitu vipi ambavyo vinaonekana na kuhisiwa na watu? Je, mmewahi kuyafikiria haya awali? Pengine hamkuyafikiria

sana, kwa hivyo wacha Nitaje hoja kadhaa muhimu. Kila mtu anajua kuhusu nadharia ya mageuko ambayo Shetani anapendekeza, siyo? Je, si hii ni sehemu ya maarifa yanayosomwa na mwanadamu? (Ndiyo.) Hivyo, Shetani kwanza anatumia maarifa kumpotosha mwanadamu, na huwafunza maarifa na mbinu yake mwenyewe. Kisha anatumia sayansi kuwapotosha wanadamu, akiamsha mvuto wao kwa maarifa, sayansi, na vitu vya ajabu, ama kwa vitu ambavyo watu wanataka kuchunguza. Vitu vifuatavyo vinavyotumiwa na Shetani kumpotosha mwanadamu ni desturi ya kitamaduni na ushirikina, na baada ya vitu hivyo, anatumia mienendo ya kijamii. Hivi vyote ni vitu ambavyo watu wanapatana navyo katika maisha yao ya kila siku na hivi vyote vinahusiana na vitu vilivyo karibu na watu, vitu wanavyoona, wanavyosikia, wanavyogusa na wanavyopitia. Mtu anaweza kusema kwamba vinazunguka kila mtu, haviwezi kutorokwa na kuepukika. Wanadamu hawana njia ya kuepuka kuathiriwa, kuambukizwa, kudhibitiwa, na kufungwa na vitu hivi; hawana nguvu za kuvisukuma mbali.

1. Jinsi Ambavyo Shetani Hutumia Maarifa Kumpotosha Mwanadamu

Kwanza tutazungumza kuhusu maarifa. Si kila mtu angechukulia maarifa kuwa kitu chema? Ama kwa kiwango cha chini kabisa, watu wanafikiri kwamba kidokezo cha neno “maarifa” ni chema badala ya hasi. Kwa hivyo mbona tunataja hapa kwamba Shetani anatumia maarifa kumpotosha mwanadamu? Si nadharia ya mageuko ni kipengele cha maarifa? Si sheria za kisayansi za Newton ni sehemu ya maarifa? Si mvuto wa dunia ni sehemu ya maarifa, siyo? (Ndiyo.) Hivyo mbona maarifa yametajwa miongoni mwa maudhui anayoyatumia Shetani kumpotosha mwanadamu? Maoni yenu hapa ni yapi? Je, maarifa yana hata chembe cha ukweli ndani yake? (La.) Kwa hivyo ni nini kiini cha maarifa? Maarifa ambayo mwanadamu anatafiti yanafunzwa kwa msingi upi? Yanalingana na nadharia ya mageuko? Si maarifa ambayo mwanadamu amepata kupitia katika uchunguzi na kujumlisha kwa msingi wa ukanaji Mungu? Kuna sehemu yoyote ya maarifa haya ambayo ina uhusiano na Mungu? Je, yanahusiana na kumwabudu Mungu? Yanahusiana na ukweli? (La.) Hivyo Shetani anatumiaje maarifa kumpotosha mwanadamu? Nimetoka tu kusema kwamba hakuna sehemu yoyote ya maarifa haya inahusiana na kumwabudu Mungu ama na ukweli. Watu wengine wanayafikiria hivi: “Yanaweza kutokuwa na chochote kuhusiana na ukweli, lakini hayawapotoshi watu.” Mnafikiri nini kuhusu haya? Ulifundishwa na maarifa kwamba furaha ya watu ilitegemea kile walichokiumba na mikono yao? Je, maarifa yaliwahi kukufunza kwamba hatima ya mwanadamu ilikuwa mikononi mwake? (Ndiyo.) Haya ni mazungumzo ya aina gani? (Ni upuuzi.) Sahihi! Ni upuuzi! Maarifa yanatatiza kujadili. Unaweza kuiweka kwa urahisi kwamba eneo la maarifa ni maarifa tu. Hili ni eneo la maarifa linalofunzwa kwa msingi wa kutomwabudu Mungu na kutokuwa na uelewa kwamba Mungu aliumba mambo yote. Watu wanaposoma aina hii ya maarifa, hawaoni Mungu anatawala mambo yote, hawaoni Mungu anaongoza ama anasimamia mambo yote. Badala yake,

wanayofanya tu ni kutafiti na kuchunguza, bila kikomo kwa sehemu hiyo ya maarifa, na kutafuta majibu kwa msingi wa maarifa. Hata hivyo, iwapo watu hawamwamini Mungu na badala yake wanatafiti tu, kamwe hawatapata majibu ya kweli, siyo? Maarifa yanakupa tu riziki, yanakupa tu kazi, yanakupa tu mapato ili usiwe na njaa, lakini kamwe hayawezi kukufanya kumwabudu Mungu, na hayatakuweka mbali na maovu. Kadiri unavyosoma maarifa, ndivyo utatamani zaidi kuasi dhidi ya Mungu, kumtafiti Mungu, kumjaribu Mungu, na kwenda kinyume na Mungu. Hivyo sasa, tunaona yapi ambayo maarifa yanawafunza watu? Yote ni falsafa ya Shetani. Je, falsafa na kanuni za kuishi zinazosambazwa na shetani miongoni mwa wanadamu potovu zina uhusiano wowote na ukweli? Hazina uhusiano wowote na ukweli na, kwa kweli, ni kinyume cha ukweli. Watu mara nyingi husema, “Maisha ni mwendo” na “Mwanadamu ni chuma, mchele ni chuma, mwanadamu huhisi anataabika kwa njaa asipokula mlo”; misemo hii ni nini? Ni uwongo, na kuisikia kunasababisha hisia ya kuchukiza. Pengine kila mtu anajua kuhusu jinsi Shetani hutumia maarifa kupotosha mwanadamu. Kwa yanayoitwa maarifa ya mwanadamu, Shetani amejaza kidogo falsafa yake ya kuishi na kufikiria kwake. Na wakati Shetani anafanya haya, Shetani anamruhusu mwanadamu kutumia kufikiria kwake, filosofia, na mtazamo wake ili mwanadamu aweze kukana uwepo wa Mungu, kukana utawala wa Mungu juu ya mambo yote na utawala juu ya hatima ya mwanadamu. Kwa hivyo, masomo ya mwanadamu yanapoendelea, na anapata maarifa zaidi, anahisi uwepo wa Mungu kuwa usio yakini, na anaweza hata kuhisi kwamba Mungu hayupo. Kwa vile Shetani ameongeza mitazamo, mawazo, na fikira kwa akili ya mwanadamu, je, si binadamu amepotoshwa na jambo hili Shetani anapoweka fikira hizi ndani ya akili yake? (Ndiyo.) Ni nini msingi wa maisha ya mwanadamu sasa? Kweli anategemea maarifa haya? La; msingi wa maisha ya mwanadamu ni fikira, mitazamo na filosofia za Shetani ambazo zimefichwa kwa maarifa haya. Hapa ndipo kiini cha upotovu wa Shetani wa mwanadamu unafanyika, hili ndilo lengo la Shetani na mbinu yake ya kumpotosha mwanadamu.

Kwanza tutazungumzia kipengele cha juujuu zaidi cha mada hii. Je, sarufi na maneno katika masomo ya lugha yaliweza kuwapotosha watu? Maneno yanaweza kupotosha watu? (La.) Maneno hayapotoshi watu; ni chombo kinachowaruhusu watu kuongea na chombo ambacho watu wanatumia kuwasiliana na Mungu. Zaidi, lugha na maneno ni jinsi ambavyo Mungu anawasiliana na watu sasa, ni vyombo, ni vya umuhimu. Moja ongeza moja ni mbili, na mbili zidisha kwa mbili ni nne; haya ni maarifa, siyo? Lakini yanaweza kukupotosha? Hii ni akili ya wote na kanuni kwa hivyo haiwezi kupotosha watu. Kwa hivyo ni maarifa gani yanayopotosha watu? Ni maarifa ambayo yamechanganywa mitazamo na fikira za Shetani, Shetani anataka kujaza mitazamo na fikira hizi ndani ya binadamu kupitia maarifa. Kwa mfano, katika insha, hakuna chochote kibaya na maneno yaliyoandikwa, lakini shida inaweza kuwa mitazamo na nia ya mwandishi alipoandika insha hiyo na pia maudhui ya fikira zake. Haya ni mambo ya kiroho—

na yanaweza kuwapotosha watu. Kwa mfano, iwapo ungekuwa ukitazama kipindi kwenye runinga, ni mambo yapi ndani yake yangeweza kubadili mtazamo wako? Je, yale yaliyosemwa na wasanii, maneno yenyewe, yangeweza kuwapotosha watu? (La.) Ni mambo yapi ambayo yangeweza kuwapotosha watu? Ingekuwa fikira na maudhui ya kiini ya kipindi, ambayo yangewakilisha mitazamo ya mwelekezi, na taarifa iliyo kwa mitazamo hii ingeshawishi mioyo na akili za watu. Siyo? Sasa mnajua Narejelea nini katika mjadala Wangu wa Shetani kutumia maarifa kuwapotosha watu. Hutaifahamu vibaya, siyo? Hivyo unaposoma riwaya ama insha tena, unaweza kutathmini iwapo fikira zilizoelezwa katika insha hiyo zinapotosha ama hazipotoshi mwanadamu ama kuchangia kwa binadamu? (Tunaweza kufanya hivyo kidogo.) Hiki ni kitu ambacho lazima kisomwe na kupitiwa polepole, si kitu kinachoeleweka kwa urahisi mara moja. Kwa mfano, unapotafiti ama kusoma sehemu ya maarifa, baadhi ya vipengele vyema vya maarifa hayo vinaweza kukusaidia kuelewa baadhi ya akili ya wote kuhusu eneo hilo, na kile ambacho watu wanapaswa kuepukana nacho. Chukua mfano wa “umeme,”—huu ni uwanja wa maarifa, siyo? Je, hutakuwa mjinga iwapo hujui kwamba kwamba umeme unaweza kuwatetemesha na kuwaumiza watu? Lakini utakapoelewa sehemu hii ya maarifa, hutakuwa na uzembe kuhusu kugusa kitu cha umeme na utajua jinsi ya kutumia umeme. Haya yote ni mambo mema. Je, sasa unaelewa kile ambacho tumekuwa tukijadili kuhusiana na jinsi maarifa yanavyowapotosha watu? Kuna aina nyingi za maarifa ambazo zinasomwa duniani na lazima mchukue wakati wenu kuzitofautisha wenyewe.

2. Jinsi ambavyo Shetani Hutumia Sayansi Kumpotosha Mwanadamu

Sayansi ni nini? Si sayansi imewekwa kwa hadhi ya juu na kuchukuliwa kuwa muhimu katika akili za karibu kila mtu? Sayansi inapotajwa, si watu wanahisi, “Hiki ni kitu ambacho watu wa kawaida hawawezi kuelewa, hii ni mada ambayo tu watafiti wa kisayansi ama wataalam wanaweza kugusia. Haina uhusiano wowote na sisi watu wa kawaida”? Je, ina uhusiano lakini? (Ndiyo.) Shetani anatumiaje sayansi kuwapotosha watu? Hatutazungumza kuhusu mambo mengine isipokuwa mambo ambayo watu mara nyingi wanapatana nayo katika maisha yao binafsi. Je, umesikia kuhusu jeni? Nyote mnalijua neno hili, siyo? Je, jeni ziligunduliwa kupitia sayansi? Jeni zinamaanisha nini hasa kwa watu? Hazifanyi watu kuhisi kwamba mwili ni kitu cha ajabu? Wakati watu wanajulishwa kwa mada hii, si kutakuwa na watu—hasa wenye kutaka kujua—ambao watataka kujua zaidi ama kutaka maelezo zaidi? Hawa watu wanaotaka kujua wataweka nguvu zao zote kwenye mada hii na wakati hawana shughuli watatafuta maelezo kwenye vitabu na Intaneti kujifunza maelezo zaidi kuihusu. Sayansi ni nini? Kuongea waziwazi, sayansi ni fikira na nadharia ya vitu ambavyo mwanadamu anataka kujua, vitu visivyojulikana, na ambavyo hawajaambiwa na Mungu; sayansi ni fikira na nadharia za siri ambazo mwanadamu anataka kuchunguza. Wigo wa sayansi ni upi? Unaweza kusema kwamba ni mpana

sana; mwanadamu hutafiti na kujifunza kila kitu ambacho anavutiwa nacho. Sayansi inahusiana na kutafiti maelezo na sheria za vitu hivi na kuweka mbele nadharia zenye kukubalika ambazo zinawafanya watu wafikirie: “Wanasayansi hawa ni wakubwa mno! Wanajua mengi na wana maarifa mengi kuelewa mambo haya!” Wanapendezwa sana na watu hao, siyo? Watu wanaotafiti sayansi, wana mitazamo ya aina gani? Hawataki kutafiti ulimwengu, kutafiti mambo ya ajabu ya maeneo ya maslahi yao? Matokeo ya mwisho ya haya ni nini? Katika baadhi ya sayansi, watu wanafikia mahitimisho yao kwa kubahatisha, na katika nyingine watu wanategemea uzoefu wa binadamu kufikia mahitimisho yao. Bado katika nyanja zingine ya sayansi, watu hufikia mahitimisho yao kutokana na uchunguzi wa kihistoria na usuli. Sivyo? Hivyo, sayansi inawafanyia nini watu? Kile sayansi inafanya ni kwamba inawaruhusu tu watu kuona vyombo katika ulimwengu wa maumbile na tu kuridhisha kutaka kujua kwa mwanadamu; haimruhusu mwanadamu kuona sheria ambazo Mungu anatumia kutawala mambo yote. Mwanadamu anaonekana kupata majibu kutoka kwa sayansi, lakini majibu hayo yanachanganya na yanaleta tu ridhaa ya muda mfupi, ridhaa ambayo inawekea moyo wa mwanadamu mipaka kwa ulimwengu wa maumbile. Mwanadamu anahisi kwamba amepata majibu kutoka kwa sayansi kwa hivyo licha ya suala litakaloibuka, wanajaribu kuthibitisha au kukubali hili kwa msingi wa mitazamo yao ya kisayansi. Moyo wa mwanadamu unamilikiwa na sayansi na kushawishiwa nayo hadi pahali ambapo mwanadamu tena hana akili ya kumjua Mungu, kumwabudu Mungu, na kuamini kwamba mambo yote yanatoka kwa Mungu na mwanadamu anapaswa kumwagalia kupata majibu. Hii si ukweli? Kadiri ambavyo mtu anaamini sayansi, anakuwa mjinga zaidi, akiamini kwamba kila kitu kina suluhisho la sayansi, kwamba utafiti unaweza kutatua chochote. Hamtafuti Mungu na haamini kwamba Yupu; hata watu wengine ambao wamemfuata Mungu kwa miaka mingi wataenda na kutafiti vimelea kwa msukumo ama kutafuta baadhi ya maelezo ili kupata jibu la suala. Mtu kama huyo haangalii masuala kwa mtazamo wa ukweli na wakati mwingi anataka kutegemea mitazamo na maarifa ya kisayansi ama majibu ya kisayansi kutatua shida; lakini hamtegemei Mungu na hamtafuti Mungu. Je, watu kama hao wana Mungu katika mioyo yao? (La.) Hata kuna watu wengine wanaotaka kutafiti Mungu kwa njia sawa na vile wanasoma sayansi. Kwa mfano, kuna wataalam wengi wa kidini walioenda kwenye mlima ambako safina ilisimama, na hivyo walithibitisha kuwepo kwa safina. Lakini katika kuonekana kwa safina hawaoni uwepo wa Mungu. Wanaamini tu hadithi na historia na haya ni matokeo ya utafiti wao wa kisayansi na utafiti wa dunia ya maumbile. Ukitafiti vitu yakinifu, viwe maikrobiolojia, falaki, ama jiografia, hutawahi kupata matokeo yanayosema kwamba Mungu yupo ama kwamba anatawala mambo yote, Kwa hivyo sayansi inamfanyia nini mwanadamu? Si inamweka mbali na Mungu? Si hii inawaruhusu watu kumtafiti Mungu? Si hii inawafanya watu kuwa na shaka zaidi kuhusu uwepo wa Mungu? (Ndiyo.) Kwa hivyo Shetani anataka kutumia vipi sayansi kumpotosha mwanadamu, na atumie mahitimisho ya

kisayansi kuwadanganya na kuwanyima watu hisia? Shetani anatumia majibu yenye maana nyingi kushikilia mioyo ya watu ili wasitafute ama kuamini uwepo wa Mungu? (Ndiyo.) Hivyo, hii ndiyo sababu tunasema ni njia moja Shetani anawapotosha watu.

3. Jinsi Ambavyo Shetani Hutumia Desturi ya Kitamaduni Kumpotosha Mwanadamu

Je, kuna mambo mengi yanayochukuliwa kuwa sehemu ya desturi ya kitamaduni? (Ndiyo.) Hii desturi ya kitamaduni inamaanisha nini? Wengine wanasema inapitishwa kutoka kwa mababu, hiki ni kipengele kimoja. Kutoka mwanzo, familia, vikundi vya makabila, na hata jamii ya binadamu imepitisha njia yao ya maisha, ama mila, misemo, na kanuni, ambazo zimeingizwa kwenye fikira za watu. Watu wanayachukulia kuwa yasiyoweza kutengwa na maisha yao. Wanayachukua mambo haya na kuyachukulia kuwa kanuni na uhai wa kutii, na hata kamwe hawataki kuyabadilisha ama kuyaacha mambo haya kwa sababu yalipitishwa kutoka kwa mababu. Kuna vipengele vingine vya desturi ya kitamaduni, kama kile kilichopitishwa na Confucius ama Mencius, na mambo waliyofunzwa watu na Utao ama Uconfucius. Je, hili si kweli? Ni vitu gani vinavyojumuishwa katika desturi ya kitamaduni? Inajumuisha likizo ambazo watu wanasherehekea? Kwa mfano: Tamasha la Majira ya machipuko, Tamasha la Taa, Siku ya Kufagia Kaburi, Tamasha la Mashua ya Joka, pamoja na Tamasha ya Zimwi na Tamasha ya Katikati ya Majira ya Kupukutika kwa Majani. Baadhi za familia hata husherehekea siku ambazo wazee wanahitimu umri fulani, ama wakati watoto wanahitimu umri wa mwezi mmoja au siku mia moja. Na kadhalika. Hizi zote ni likizo za desturi. Je, hakuna desturi ya kitamaduni katika likizo hizi? Ni nini kiini cha desturi ya kitamaduni? Kina chochote cha kufanya na kumwabudu Mungu? Kina chochote cha kufanya na kuwaambia watu kuweka ukweli katika vitendo? Kuna likizo zozote za watu kutoa sadaka kwa Mungu, kwenda kwa madhabahu ya Mungu na kupokea mafunzo Yake? Kuna likizo kama hizi? (La.) Watu hufanya nini katika likizo hizi zote? Katika nyakati za sasa zinaonekana kuwa hafla za kula, kunywa, na kujiburudisha. Ni nini chanzo cha desturi ya kitamaduni? Desturi ya kitamaduni imetoka kwa nani? (Shetani.) Imetoka kwa Shetani. Katika usuli wa hizi likizo za desturi, Shetani anaingiza mambo ndani ya mwanadamu, haya ni mambo gani? Kuhakikisha kwamba watu wanakumbuka mababu zao, hili ni mojawapo ya mambo haya? Kwa mfano, wakati wa Tamasha la Kufagia Kaburi watu husafisha makaburi na kutoa sadaka kwa mababu zao, hivyo watu hawatasahau mababu zao. Pia, Shetani anahakikisha kwamba watu wanakumbuka kuwa wazalendo, kama katika Tamasha la Mashua ya Joka. Je, Tamasha la Katikati ya Majira ya Kupukutika kwa Majani? (Kupatana kwa familia.) Ni nini usuli wa kupatana kwa familia? Sababu zake ni nini? Ni kuwasiliana na kuunganika kihisia. Bila shaka, iwapo ni kusherehekea Mkesha wa Mwaka Mpya wa Mwezi ama Tamasha la Taa, kuna njia nyingi za kuelezea sababu za usuli. Haijalishi mtu anaelezea sababu iliyo nyuma yazo, kila moja ni njia ya Shetani ya kuingiza filosofia yake na kufikiria kwake kwa watu, ili waweze

kupotea kutoka kwa Mungu na wasijue kwamba kuna Mungu, na kwamba watoe sadaka ama kwa mababu zao au Shetani, ama kwamba ni udhuru wa kula, kunywa na kujifurahisha kwa ajili ya matamano ya mwili. Kila ya likizo hizi inaposherehekeka, fikira na mitazamo ya Shetani yanapandwa kwa kina ndani ya akili za watu na hata hawajui. Wakati watu wanafika umri wa kati ama zaidi, fikira na mitazamo hii ya Shetani tayari yamekita mizizi ndani sana ya mioyo yao. Zaidi, watu wanafanya juhudi zao kabisa kueneza fikira hizi, ziwe sahihi ama si sahihi, kwa kizazi kifuatacho bila wasiwasi pasipo kuchagua. Sivyo? (Ndiyo.) Ni jinsi gani desturi hii ya kitamaduni na likizo hizi zinapotosha vipi watu? Unajua? (Watu wanawekewa mipaka na kufungwa na kanuni za hizi desturi kana kwamba hawana muda ama nguvu kumtafuta Mungu.) Hiki ni kipengele kimoja. Kwa mfano, kila mtu anasherehekea wakati wa Mwaka Mpya wa Mwezi, usingesherehekea, hungehisi huzuni? Je, kuna miiko yoyote ambayo unapaswa kushikilia? Hungehisi, “Sikusherehekea Mwaka Mpya. Siku hii ya Mwaka Mpya wa Mwezi ilikuwa mbaya sana; mwaka huu wote utakuwa mbaya”? Si ungehisi kutokuwa na utulivu na kuogopa kiasi? Kuna hata watu wengine ambao hawajatoa sadaka kwa mababu zao kwa miaka mingi na ghafla wamekuwa na ndoto ambapo mtu aliyekufa anawaomba pesa, watahisi nini ndani yao? “Inahuzunisha kwamba huyu mtu aliyekufa anahitaji pesa ya kutumia! Nitawachomea baadhi ya pesa ya karatasi, nisipo hiyo hakika haitakuwa sawa. Sisi tunaoishi tunaweza kupatana na shida kidogo nisipochoma baadhi ya pesa ya karatasi, ni nani anayeweza kusema wakati janga litatokea?” Daima watakuwa na wingu hili dogo la hofu na wasiwasi katika mioyo yao. Ni nani anayewapa wasiwasi? (Shetani.) Shetani huleta wasiwasi. Si hii ndiyo njia moja ambayo Shetani anampotosha mwanadamu? Anatumia mbinu na udhuru mbalimbali ili kukudhibiti, kukutishia, kukufunga, hadi kiasi kwamba unachanganyikiwa na kumkubali na kumnyenyekea; hivi ndivyo Shetani anampotosha mwanadamu. Nyakati nyingi ambapo watu ni wanyonge ama hawaelewi vyema hali ilivyo, wanaweza bila kutaka, kufanya kitu kwa njia iliyochanganyikiwa, yaani, wanaanguka chini ya mshiko wa Shetani bila kusudi na wanaweza kufanya kitu bila kusudi na wasijue wanafanya nini. Hii ni njia ambayo Shetani anampotosha mwanadamu. Hata kuna watu wachache sasa ambao wanasita kuachana na desturi za kitamaduni ambazo zimekita mizizi, ambao hawawezi kuziacha kabisa. Ni hasa wakati ni wanyonge na wasipoonyesha hisia ndipo wanataka kusherehekea likizo za aina hizi na wanataka kukutana na Shetani na kumridhisha Shetani tena, ili kuifariji mioyo yao. Ni nini usuli wa desturi hizi za kitamaduni? Mkono mweusi wa Shetani unavuta nyuzi nyuma ya pazia? Asili ovyo ya Shetani inatawala na kudhibiti vitu? Shetani anadhibiti hivi vitu vyote? (Ndiyo.) Wakati watu wanaishi katika desturi ya kitamaduni na kusherehekea likizo za desturi za aina hizi, tunaweza kusema kwamba haya ni mazingira ambapo wanadanganywa na kupotoshwa na Shetani, na zaidi ya hayo kwamba wana furaha kupumbazwa na kupotoshwa na Shetani? (Ndiyo.) Hiki ni kitu ambacho nyinyi nyote mnakiri, ambacho nyote mnakijua.

4. Jinsi Ambavyo Shetani Hutumia Ushirikina Kumpotosha Mwanadamu

Mnalijua neno “ushirikina,” siyo? Kuna usawa unaopatana kati ya ushirikina na desturi ya kitamaduni, lakini hatutazungumza kuhusu huo leo, badala yake Nitajadili unaokabiliwa mara nyingi: uganga, uaguzi, kuchoma ubani, na kuabudu Buddha. Watu wengine wanafanya uganga, wengine wanaabudu Buddha na kuchoma ubani, ilhali wengine wanabashiriwa ama wanaambiwa bahati zao kwa kumruhusu mtu kusoma vipengele vya nyuso zao. Wangapi kati yenu wameambiwa bahati zao ama wamesomwa uso? Hiki ni kitu ambacho watu wengi wanataka, siyo? (Ndiyo.) Mbona hivyo? Watu wanapata faida ya aina gani kutoka kwa uaguzi na uganga? Wanapata ridhaa ya aina gani kutoka kwa hayo? (Udadisi.) Je, ni udadisi tu? Hiyo si lazima iwe hivyo, jinsi nionavyo mimi. Lengo la ubashiri na upigaji ramli ni nini? Mbona ufanyiwe? Si kwa ajili ya kuona siku za baadaye? Watu wengine wanasomwa nyuso zao ili kutabiri siku za baadaye, wengine wanafanya hivyo ili kuona iwapo watakuwa na bahati nzuri au la. Wengine wanafanya hivyo ili kuona vipi ndoa zao zitakuwa, na bado wengine wanafanya hivyo kuona bahati itakayoletwa na mwaka ulio mbele. Watu wengine wanasomwa nyuso zao kuona matarajio yao na yale ya wana na binti zao yatakuwa vipi, na wanabiashara wengine wanafanya hivyo kuona watatengeneza pesa ngapi ili waweze kupata mwongozo kwa kile wanachopaswa kufanya. Je, ni kuridhisha udadisi tu? Wakati watu wanasomwa nyuso zao ama kufanya vitu vya aina hii, ni kwa faida ya siku zao za baadaye binafsi na wanaamini kwamba haya yote yanahusiana kwa karibu na hatima zao. Je, kuna yoyote katika mambo haya yaliyo ya manufaa? (La.) Mbona si ya manufaa? Si kitu kizuri kujua kidogo kuhusu mambo hayo? Hii inakusaidia kujua wakati shida inaweza kutokea, ili uweze kuiepuka kama ulikuwa unajua kuihusu awali, siyo? Kupigiwa ramli kunaweza kukuruhusu kuongozwa kuhusiana nako, ili mwaka ulio mbele uweze kuwa mzuri na unaweza kuwa tajiri ukifanya biashara. Hili ni ya manufaa? Liwe ni la manufaa au la halituhusu, na ushirika wetu leo hautahusisha mada hii. Shetani anatumiaje ushirikina kumpotosha mwanadamu? Watu wote wanataka kujua majaliwa yao, hivyo Shetani anatumia udadisi wao kuwashawishi. Watu wanashiriki katika ubashiri, upigaji ramli na kusoma uso ili kujua kile kitakachowafanyikia katika siku zijazo na ni njia ya aina gani iliyo mbele yao. Hata hivyo, mwishowe, majaliwa na matarajio ambavyo watu hawa wana wasiwasi navyo sana viko mikononi mwa nani? (Mikononi mwa Mungu.) Vitu hivi vyote vimo katika mikono ya Mungu. Kwa kutumia mbinu hizi, Shetani anataka watu wajue nini? Shetani anataka kutumia kusoma uso na uaguzi ili kuwaambia watu kwamba anajua bahati zao mbeleni, na Shetani anataka kuwaambia watu kwamba anajua vitu hivi na anavidhibiti. Shetani anataka kutumia fursa hii na kutumia mbinu hizi kudhibiti watu, ili kwamba watu wanamwekea imani isiyoweza kutambua na kutii kila neno lake. Kwa mfano, ukisomwa uso, mwaguzi akifunga macho yake na kukwambia kila kitu ambacho kimekufanyikia katika miongo michache

iliyopita kwa uwazi kamili, ungehisi vipi ndani yako? Ghafla ungehisi, “Yuko sahihi sana! Sijawahi kumwambia yeyote maisha yangu ya nyuma, alijuaje kuyahusu? Nimependezwa sana na huyu mwaguzi!” Haitakuwa vigumu sana kwa Shetani kujua maisha yako ya nyuma, siyo? Mungu amekuongoza hadi leo, na Shetani pia amewapotosha watu wakati huo wote na amekufuata. Kupita kwa miongo kwako si chochote kwa Shetani na si vigumu kwake kujua vitu hivi. Wakati unajua kwamba alichosema Shetani ni sahihi, si unampa moyo wako? Siku zako za baadaye na bahati yako, si unategemea udhibiti wake? Papo hapo, moyo wako utahisi heshima ama ustahi kwake, na kwa watu wengine, nafsi zao pengine tayari zimenyakuliwa naye. Na utamwuliza mwaguzi mara moja: “Napaswa kufanya nini baada ya hapa? Napaswa kuepukana na nini mwaka ujao? Ni vitu gani ambavyo sipaswi kufanya?” Na kisha atasema hupaswi kwenda pale, hupaswi kufanya hili, usivae nguo za rangi fulani, hupaswi kwenda pahali kama hapo na hapo unapaswa kufanya mambo fulani zaidi.... Si utatia vyote anavyosema moyoni mara moja? Ungevikariri haraka kuliko neno la Mungu. Mbona ungevikariri haraka hivyo? Kwa sababu ungetaka kumtegemea Shetani kwa sababu ya bahati njema. Si hapa ndipo anaunyakua moyo wako? Wakati maneno yake yanakuwa ukweli kama alivyotabiri, hungetaka kurudi nyuma kwake na kujua ni bahati gani mwaka unaokuja utaleta? (Ndiyo.) Utafanya chochote Shetani anakwambia ufanye na utaepukana na vitu anakwambia uepukane navyo, si unatii vyote anavyosema? Utajipata katika kumbatio lake haraka sana, upotoshwe, na kudhibitiwa naye. Hii inafanyika kwa sababu unaamini anachosema ni ukweli na kwa sababu unaamini kwamba anajua kuhusu maisha yako ya nyuma, maisha yako ya sasa, na vitu ambavyo siku za badaye zitaleta. Hii ni mbinu Shetani anatumia kudhibiti watu. Lakini kwa kweli, ni nani aliye katika udhibiti? Ni Mungu Mwenyewe, si Shetani. Shetani anatumia tu hila zake hapa kudanganya watu wajinga, kuwadanganya watu wanaoona tu ulimwengu wa maumbile kumwamini na kumtegemea. Kisha, wataanguka katika mshiko wa Shetani na kutii kila neno lake. Lakini Shetani wakati wowote hupunguza jitihada watu wanapotaka kumwamini na kumfuata Mungu? Shetani hapunguzi jitihada. Katika hali hii, watu kweli wanaanguka katika mshiko wa Shetani? (Ndiyo.) Tunaweza kusema kwamba tabia ya Shetani hapa haina haya hata kidogo? (Ndiyo.) Mbona tungenesema hivyo? Hizi ni mbinu za ulaghai na zinadanganya. Shetani hana haya na anawadanganya watu kufikiria kwamba anadhibiti kila kitu chao na kuwadanganya watu kufikiria kwamba anadhibiti hatima zao. Hii inawafanya watu wajinga kuja kumtii kabisa na anawadanganya na sentensi moja ama mbili tu na katika kuchanganyikiwa kwao, watu wanasujudu mbele yake. Hivyo, Shetani anatumia mbinu za aina gani, anasema nini kukufanya umwamini? Kwa mfano, pengine hujamwambia Shetani idadi ya watu katika familia yako, lakini anaweza kusema kuna watu wangapi katika familia yako, na umri wa wazazi wako na watoto wako. Iwapo ulikuwa na tuhuma na shaka zako mwanzoni, hutahisi kwamba anaaminika zaidi kidogo baada ya kusikia hayo? Shetani kisha anaweza kusemajinsi kazi imekuwa ngumu kwako hivi karibuni, kwamba

wakubwa wako hawakupi utambuzi unaostahili na daima wanafanya kazi dhidi yako na kadhalika. Baada ya kuyasikia hayo, ungefikiri, “Hiyo ni sahihi kabisa! Mambo hayajakuwa yakienda vizuri kazini.” Hivyo ungemwamini Shetani zaidi kidogo. Kisha angesema kitu kingine kukudanganya, kukufanya umwamini hata zaidi. Kidogo kidogo, utajipata huwezi kupinga ama kuwa na tuhuma kwake tena. Shetani anatumia tu hila chache zisizo na maana, hata ndogo zisizojalisha, kukufadhaisha. Unapofadhaishwa, hutaweza kupata njia zako, hutajua kile cha kufanya, na utanza kufuata kile Shetani anasema. Hii ni mbinu ya “ah nzuri sana” anayotumia Shetani kumpotosha mwanadamu pahali unapoingia katika mtogo wake bila kusudi na unashawishiwa naye. Shetani anakwambia mambo machache ambayo watu wanafikiria kuwa mambo mazuri, na kisha anakwambia kile cha kufanya na kile cha kuepuka. Hivi ndivyo unavyodanganywa bila kujua. Punde unapoingia mtegoni mwake, mambo yatakwendea mrama; daima utakuwa ukifikiria kile alichosema Shetani na kile alichokwambia ufanye, na bila kujua utamilikiwa naye. Mbona hivi? Ni kwa sababu wanadamu hawana ukweli na hivyo hawawezi kusimama dhidi ya majaribu na ushawishi wa Shetani. Wanapokabiliwa na uovu, udanganyifu, usaliti, na kijicho cha Shetani, wanadamu ni wajinga sana, ni wachanga na wanyonge, siyo? Si hii ni mojawapo ya njia ambayo Shetani anampotosha mwanadamu? (Ndiyo.) Mwanadamu anadanganywa na kulaghaiwa bila kusudi, kidogo kidogo, kupitia mbinu mbalimbali za Shetani, kwa sababu hawana uwezo wa kutofautisha kati ya mema na hasi. Hawana kimo hiki, na uwezo wa kumshinda Shetani.

5. Jinsi Ambavyo Shetani Hutumia Mienendo ya Kijamii Kumpotosha Mwanadamu

Mienendo ya kijamii ilianza lini? Je, ni kitu kipya? Mtu anaweza kusema kwamba mienendo ya kijamii ilianza wakati Shetani alipoanza kuwapotosha watu. Mienendo ya kijamii inajumuisha nini? (Mtindo wa mavazi na vipodozi.) Hiki ni kitu ambacho watu mara nyingi wanakutana nacho. Mtindo wa mavazi, mtindo wa kisasa na mienendo, hiki ni kipengele kidogo. Kuna kingine zaidi? Je, misemo maarufu ambayo watu wanapenda kusema inahesabika pia? Je, pia mitindo ya maisha ambayo watu wanataka inahesabika? Je, nyota wa muziki, watu mashuhuri, majarida, na riwaya ambazo watu hupenda zinahesabika? (Ndiyo.) Katika akili zenu, ni kipengele kipi cha mienendo hii kinaweza kumpotosha mwanadamu? Ni mienendo ipi inawavutia sana? Watu wengine husema: “Sisi sote tumefikia umri fulani, tuko katika miaka ya, hamsini, sitini, sabini ama themanini ambapo hatuwezi kufaa katika mienendo hii na haituvutii tena.” Je, hii ni sahihi? Wengine husema: “Hatufuati watu mashuhuri, hicho ni kitu ambacho vijana walio katika umri wa ishirini wanafanya; pia hatuvai nguo za mitindo ya kisasa, hicho ni kitu ambacho watu wanaojali sura wanafanya.” Kwa hivyo ni ipi kati ya hii inaweza kuwapotosha? (Misemo maarufu.) Je, hii misemo maarufu inaweza kuwapotosha watu? Huu ni msemu mmoja, na mnaweza kuona iwapo unawapotosha watu au la, “Pesa inaifanya dunia

izunguke”; huu ni mtindo? Ikilinganishwa na mitindo ya mavazi na chakula mliyotaja, sihuu ni mbaya zaidi? “Pesa inaifanya dunia izunguke” ni falsafa ya Shetani, na inaenea miongoni mwa wanadamu wote, katika kila jamii ya binadamu. Mnaweza kusema kwamba ni mwenendo kwa sababu umewekwa ndani ya moyo wa kila mtu. Tangu mwanzo kabisa, watu hawakuukubali msemu huu, lakini kisha waliukubali bila kusema walipokutana na maisha halisi, na wakaanza kuhisi kwamba maneno haya kweli yalikuwa ya kweli. Je, huu si mchakato wa Shetani kumpotosha mwanadamu? Pengine watu hawaelewi msemu huu kwa kiwango sawa, lakini kila mtu ana viwango tofauti vya tafsiri na kukiri kwa msemu huu kutokana na mambo ambayo yamefanyika karibu nao na uzoefu wao binafsi, siyo? Licha ya kiwango cha uzoefu mtu anao na msemu huu, ni nini athari mbaya unaweza kuwa nao katika moyo wa mtu? Kitu fulani kinafichuliwa kupitia tabia ya binadamu ya watu katika dunia hii, ikiwemo kila mmoja wenu. Hiki kinafasiriwa vipi? Ni ibada ya pesa. Ni vigumu kutoa hili kwa moyo wa mtu? Ni vigumu sana! Inaonekana kwamba upotovu wa Shetani kwa mwanadamu ni kamili kabisa! Hivyo baada ya Shetani kutumia mwenendo huu kuwapotosha watu, unaonyeshwa vipi kwao? Hamhisi kwamba hamtaishi katika dunia hii bila pesa yoyote, kwamba hata siku moja haiwezekani? Hadhi ya watu inatokana na kiasi cha pesa wako nayo na pia heshima yao. Migongo ya maskini imekunjwa kwa aibu, ilhali matajiri wanafurahia hadhi zao za juu. Wanatenda kwa njia ya kujigamba na wana majivuno, wakiongea kwa sauti kubwa na kuishi kwa kiburi. Msemu na mwenendo huu unaleta nini kwa watu? Si watu wengi wanaona kupata pesa kunastahili gharama yoyote? Si watu wengi hutoa Heshima na uadilifu wao wakitafula pesa zaidi? Si watu wengi hupoteza fursa ya kufanya wajibu wao na kumfuata Mungu kwa sababu ya pesa? Si hii ni hasara kwa watu? (Ndiyo.) Si Shetani ni mbaya kutumia mbinu hii na msemu huu kumpotosha mwanadamu kwa kiwango kama hicho? Si hii ni hila yenye kijicho? Unaposonga kutoka kuukataa huu msemu maarufu hadi mwishowe kuukubali kama ukweli, moyo wako unaanguka kabisa chini ya mshiko wa Shetani, na hivyo unakuja kuishi naye bila kusudi. Msemu huu umekuathiri kwa kiwango kipi? Unaweza kujua njia ya ukweli, na unaweza kujua ukweli, lakini huna nguvu ya kuufuatilia. Unaweza kujua kwa hakika kwamba maneno ya Mungu ni ukweli, lakini huko radhi kulipa gharama au kuteseka ili kupata ukweli. Badala yake, kwako, ni afadhali utoe siku zako za baadaye na kudura yako kwenda kinyume na Mungu hadi mwisho kabisa. Licha ya kile Mungu anasema, licha ya kile Mungu anafanya, licha ya kiasi unagundua kwamba upendo wa Mungu kwako ni wa kina na mkubwa, bado ungeendelea kwa njia hiyo kwa ukaidi na kulipa gharama ya msemu huu. Hiyo ni kusema huu msemu tayari unadhibiti tabia na fikira zako, na unaona afadhali hatima yako idhibitiwe na msemu huu kuliko kuyatoa yote. Watu wanafanya hivi, wanadhibitiwa na msemu huu na kutawaliwa nao. Hii si athari ya Shetani kumpotosha mwanadamu? Hii si filosofia na tabia potovu ya Shetani ikikita mizizi kwa moyo wako? Ukifanya hivyo, si Shetani amefikia lengo lake? (Ndiyo.) Unaona jinsi Shetani

amempotosha mwanadamu kwa njia hii? Unaweza kumhisi? (La.) Hukumwona wala kumhisi. Je, unaona uovu wa Shetani hapa? Shetani humpotosha mwanadamu wakati wote na pahali pote. Shetani anaifanya isiwezekane kwa mwanadamu kujilinda dhidi ya upotovu huu na anamfanya mwanadamu awe mnyonge kwake. Shetani anakufanya ukubali fikira zake, mitazamo yake na mambo maovu yanayotoka kwake katika hali ambapo huna kusudi na huna utambuzi wa kile kinachokufanyikia. Watu wanakubali kikamilifu vitu hivi na hawavibagui. Wanapenda sana vitu hivi na kuvishikilia kama hazina, wanaviacha vitu hivi viwatawale na kuwachezea, na hivi ndivyo upotovu wa Shetani kwa mwanadamu unakuwa wa kina zaidi tena zaidi.

Shetani hutumia mbinu hizi nyingi kumpotosha mwanadamu. Mwanadamu ana maarifa na baadhi ya nadharia za kisayansi, mwanadamu anaishi na ushawishi wa desturi ya kitamaduni, na kila mtu ni mrithi na msambazaji wa desturi ya kitamaduni. Mwanadamu ataendeleza desturi ya kitamaduni aliyopewa kutoka kwa Shetani na pia kutenda pamoja na mienendo ya kijamii ambayo Shetani anawapa wanadamu. Binadamu hawezi kutengana na Shetani, kushiriki na kile ambacho Shetani anafanya wakati wote, kukubali uovu, udanganyifu, kijicho na kiburi chake. Mwanadamu alipomiliki tabia hizi za Shetani, amekuwa na furaha ama huzuni kuishi miongoni mwa binadamu hawa wapotovu? (Huzuni.) Mbona unasema hivyo? (Kwa sababu binadamu amefungwa na anadhibitiwa na vitu hivi vipotovu, anaishi dhambini na amegubikwa na mapambano makali). Watu wengine huvaa miwani, wakionekana kuwa werevu; wanaweza kuzungumza kwa heshima sana, kwa ufasaha na mantiki, na kwa sababu wamepitia vitu vingi sana, wanaweza kuwa wenye uzoefu sana na wastaarabu. Wanaweza kuzungumza kwa undani kuhusu masuala makubwa na madogo; wanaweza pia kutathmini uhalisi na mantiki ya vitu. Wengine wanaweza kuangalia tabia na kuonekana kwa watu hawa, na vile vile tabia, ubinadamu, mwenendo, na kadhalika, na wasione kosa lolote katika haya. Watu kama hao wanaweza hasa kuzoea mitindo ya sasa ya kijamii. Ingawa mtu huyu anaweza kuwa mzee, kamwe hayuko nyuma ya nyakati na kamwe si mzee sana kufunzwa. Juujuu, hakuna anayeweza kupata dosari kwake, lakini ndani amepotoshwa na Shetani kabisa na kikamilifu. Juujuu hakuna chochote kibaya, yeye ni mpole, ni muungwana, anayo maarifa na maadili fulani; ana uadilifu na vitu anavyojua vinalingana na vile wanavyojua vijana. Hata hivyo, kuhusu asili na kiini chake, mtu huyu ni mfano kamili na unaoishi wa Shetani, ana usawa kabisa na Shetani. Hili ni “tunda” la upotovu wa Shetani kwa mwanadamu. Kile Nilichosema kinaweza kuwaumiza, lakini chote ni ukweli. Maarifa ambayo mwanadamu anasoma, sayansi anayoelewa, na mbinu anazochagua kuingiliana na mienendo ya jamii, bila ubaguzi, ni vyombo vya upotovu wa Shetani. Huu ni ukweli kabisa. Kwa hivyo, mwanadamu anaishi miongoni mwa tabia ambayo imepotoshwa kabisa na Shetani na mwanadamu hana njia ya kujua utakatifu wa Mungu ni nini na kiini cha Mungu ni nini. Hii ni kwa sababu juujuu mtu hawezi kupata dosari kwa njia ambazo Shetani

anampotosha mwanadamu; hakuna anayeweza kuamua kutoka kwa tabia ya mtu kwamba kuna chochote kibaya. Kila mtu anaendelea na kazi yake kwa kawaida na kuishi maisha ya kawaida; wanasoma vitabu na magazeti kwa kawaida, wanasoma na kuzungumza kwa kawaida. Watu wengine wamejifunza maadili machache na ni wazuri katika kuzungumza, ni wenye kuelewa na ni wazuri, ni wenye kusaidia wengine, na hawajihusishi katika ugomvi wa mambo madogo madogo au kuwadhulumu watu wengine. Hata hivyo, tabia yao iliyopotoka ya kishetani imekita mizizi ndani yao; kiini hiki hakiwezi kubadilishwa kwa kutegemea juhudi za nje. Mwanadamu hana uwezo wa kujua utakatifu wa Mungu kwa sababu ya kiini hiki, na licha ya kiini cha utakatifu wa Mungu kuwekwa wazi kwa mwanadamu, mwanadamu hakichukulii kwa umakini. Hii ni kwa sababu Shetani tayari amemiliki kabisa hisia, fikira, mitazamo, na mawazo ya mwanadamu kupitia njia mbalimbali. Huu umiliki na upotovu si wa muda mfupi ama wa mara kwa mara; upo kila mahali na kila wakati. Hivyo, watu wengi mno ambao wamemwamini Mungu kwa miaka mitatu au minne hata miaka sita na saba, bado wanachukulia mawazo, fikira na falsafa hivi za uovu ambazo Shetani aliweka ndani yao kama vitu vya thamani, na hawawezi kuviachilia. Kwa sababu mwanadamu ameukubali uovu, kiburi, na mambo kutoka kwa asili ya kijicho ya Shetani, bila kuepukika kwa mahusiano ya ana kwa ana ya mwanadamu mara nyingi kuna migogoro, mara nyingi kuna magombano na kutokuwa na uwiano, mambo ambayo yameumbwa kwa sababu ya asili ya kiburi ya Shetani. Iwapo Shetani angempa mwanadamu vitu vyema—kwa mfano, iwapo Uconfucius na Utao wa desturi ya kitamaduni ambayo mwanadamu alikubali ilichukuliwa kuwa vitu vizuri—watu wa aina sawa wanapaswa kuweza kupatana na wengine baada ya kukubali vitu hivyo. Hivyo mbona kuna mgawanyiko mkubwa kati ya watu waliokubali vitu sawa? Mbona hivyo? Ni kwa sababu viti hivi vimetoka kwa Shetani na Shetani husababisha mgawanyiko miongoni mwa watu. Vitu ambavyo Shetani anapatiana, bila kujali jinsi vinavyoonekana kuwa vya heshima na vikubwa juujuu, vinamletea mwanadamu na vinaleta katika maisha ya mwanadamu kiburi pekee, na si chochote ila udanganyifu wa asili ovyo ya Shetani. Sivyoy? Mtu ambaye angeweza kujificha, kumiliki maarifa mengi, ama kuwa na malezi mazuri angekuwa na wakati mgumu kusitiri tabia yao potovu ya kishetani. Hiyo ni kusema, haijalishi mtu huyu atajificha kwa njia ngapi, kama ulimfikiri kuwa mtakatifu, ama kama ulifikiri ni mkamilifu, ama kama ulifikiri ni malaika, haijalishi ulifikiri ni mtu safi vipi, maisha yake yangekuwaje nyuma ya pazia? Utaona asili ipi katika ufunuo wa tabia yake? Bila shaka ungeona asili ovyo ya Shetani. Mtu anaweza kusema hivyo? (Ndiyo.) Kwa mfano, tuseme mnamjua mtu wa karibu nanyi ambaye mlifikiri kuwa mtu mzuri, ama ulimfikiri kuwa mtu mzuri, pengine mtu uliyemwabudu kama Mungu. Kwa kimo chako cha sasa, unawafikiri vipi? Kwanza, unaangalia iwapo mtu wa aina hii ana ama hana ubinadamu, iwapo ni mwaminifu, iwapo ana upendo wa kweli kwa watu, iwapo maneno na vitendo vyao vinafaidi na kusaidia wengine. (La.) Yaitwayo wema, upendo na uzuri unaofichuliwa hapa, ni nini kweli?

Yote ni uongo, yote ni sura ya kinafiki. Hii sura ya kinafiki ya nyuma ya pazia ina madhumuni maovu ya chinichini: Ni ya kumfanya mtu huyo apendwe na kuabudiwa kama Mungu. Je, mnaona jambo hili kwa dhahiri? (Ndiyo.)

Mbinu ambazo Shetani anatumia kuwapotosha watu zinaletea nini binadamu? Kuna chochote chema kuzihusu? Kwanza, mwanadamu anaweza kutofautisha kati ya mema na mabaya? Je, unaweza kusema kwamba katika dunia hii ni sahihi, iwe ni mtu mashuhuri au mtu mkubwa, au jarida fulani au toleo fulani, ndivyo viwango ambavyo wanatumia kupima iwapo kitu fulani ni chema ama kiovu, na chema ama kibaya? Tathmini zao za matukio na watu ni za haki? Kuna ukweli ndani ya tathmini hizi? Je, dunia hii ama binadamu huu unatathmini vitu vyema na hasi kulingana na kiwango cha ukweli? (La.) Mbona watu hawana uwezo huo? Watu wamesoma maarifa mengi na wanajua mengi kuhusu sayansi, uwezo wao si mkubwa kutosha? Mbona hawawezi kutofautisha kati ya vitu vyema na hasi? Mbona hivi? (Kwa sababu watu hawana ukweli; sayansi na maarifa si ukweli.) Kila kitu Shetani anauletea binadamu ni uovu na upotovu na hakina ukweli, uhai, na njia. Na uovu na upotovu ambao Shetani anamletea mwanadamu, unaweza kusema kwamba Shetani ana upendo? Unaweza kusema kwamba mwanadamu ana upendo? Watu wengine wanaweza kusema: “Huko sahihi, kuna watu wengi duniani kote wanaosaidia maskini na watu wasio na makazi. Si hao ni watu wazuri? Pia kuna mashirika ya hisani ambayo hufanya kazi nzuri; je, si kazi yote wanayofanya ni kazi nzuri?” Utasema nini kuhusu hayo? Shetani anatumia mbinu na nadharia mbalimbali kumpotosha mwanadamu; huu upotovu wa mwanadamu ni dhana isiyo dhahiri? La, siyo dhahiri. Shetani pia anafanya vitu vingine vya utendaji, na pia anakuza mtazamo au nadharia katika dunia hii na katika jamii. Katika kila nasaba na katika kila kipindi cha historia, anakuza nadharia na kuingiza baadhi ya fikira ndani ya wanadamu. Fikira na nadharia hizi polepole zinakita mizizi katika mioyo ya watu, na kisha watu wanaanza kuishi kwa nadharia na fikira hizi. Punde wanapoishi kulingana na mambo haya, si wanakuwa Shetani bila kusudi? Si watu wako kitu kimoja na Shetani? Wakati watu wamekuwa kitu kimoja na Shetani, ni nini mtazamo wao kwa Mungu mwishowe? Si ni mtazamo sawa ambao Shetani anao kwa Mungu? Hakuna anayethubutu kukubali haya, siyo? Ni ya kutisha sana! Mbona Nasema kwamba asili ya Shetani ni ovu? Hii inaamuliwa na kuchambuliwa kulingana na kile Shetani amefanya na vitu ambavyo Shetani amefichua; si bila ustahili kusema kwamba Shetani ni mwovu. Iwapo Ningesema tu kwamba Shetani ni mwovu, mngefikiri nini? Mngefikiri, “Bila shaka Shetani ni mwovu.” Hivyo nitakuuliza: “Ni kipengele kipi cha Shetani ni ovu?” Ukisema: “Shetani kumpinga Mungu ni uovu,” bado hutakuwa ukizungumza kwa uwazi. Sasa tumesema mambo maalum kwa njia hii; je, mna uelewa kuhusu maudhui maalum ya kiini cha uovu wa Shetani? (Ndiyo.) Ikiwa unaweza kuona waziwazi asili ovu ya Shetani, basi utaona hali zako mwenyewe. Je, kuna uhusiano

wowote kati ya vitu hivi viwili? Je, hili ni jambo lenye manufaa kwako au la? (Ni lenye manufaa). Ninaposhiriki kuhusu kiini cha utakatifu wa Mungu, ni muhimu Niwe na ushirika kuhusu kiini ovu cha Shetani. Maoni yako kuhusu hilo ni yapi? (Ndiyo, ni muhimu.) Mbona? (Uovu wa Shetani unauweka utakatifu wa Mungu katika pumziko.) Je, hivyo ndivyo ilivyo? Hii ni sahihi kwa kiasi fulani, ikichukuliwa kwamba bila uovu wa Shetani, watu hawangejua kwamba Mungu ni mtakatifu; ni sahihi kusema hivi. Hata hivyo, ukisema kwamba utakatifu wa Mungu upo tu kwa sababu ya tofauti yake na uovu wa Shetani, hii ni sahihi? Hii namna ya kujua ukweli kwa majadiliano si sahihi. Utakatifu wa Mungu ni kiini cha asili cha Mungu; hata ingawa Mungu anaufichua kupitia matendo Yake, hili bado ni onyesho asili la kiini cha Mungu na ni kiini cha asili cha Mungu; daima kimekuwepo na ni cha kiasili na cha ndani cha Mungu Mwenyewe, ingawa mwanadamu hawezi kukiona. Hii ni kwa sababu mwanadamu anaishi katikati ya tabia potovu ya Shetani na chini ya ushawishi wa Shetani, na hawajui kuhusu utakatifu, sembuse maudhui maalum ya utakatifu wa Mungu. Hivyo, ni muhimu kweli kwamba tushiriki kwanza kuhusu kiini ovu cha Shetani? (Ndiyo, ni muhimu.) Watu wengine wanaweza kuonyesha baadhi ya shaka kama, “Unashiriki kuhusu Mungu Mwenyewe, mbona Unazungumza daima kuhusu jinsi Shetani anawapotosha watu na jinsi asili ya Shetani ni ovu?” Sasa umeyaweka mapumzikoni mashaka haya, siyo? Wakati watu wana utambuzi wa uovu wa Shetani na wakati wana ufafanuzi sahihi wa uovu, wakati watu wanaweza kuona wazi maudhui maalum na udhihirisho wa uovu, chanzo na kiini cha uovu—wakati utakatifu wa Mungu unajadiliwa sasa—watu basi watatambua wazi, ama kuufahamu wazi kama utakatifu wa Mungu, kama utakatifu wa kweli. Nisipojadili uovu wa Shetani, watu wengine wataamini kimakosa kwamba kitu fulani ambacho watu wanafanya katika jamii ama miongoni mwa watu—ama kitu fulani katika dunia hii—kinaweza kuhusiana na utakatifu. Si mtazamo huu ni wa makosa? (Ndiyo.)

Hivi, Nimeshiriki kuhusu kiini cha Shetani. Mmefikia uelewa upi wa utakatifu wa Mungu kupitia uzoefu wenu wa miaka ya hivi karibuni, kutokana na nyinyi kuona neno la Mungu na kutokana na kupitia kazi Yake? Endelea, na uzungumzie. Si lazima utumie maneno yanayofurahisha sikio, zungumza tu kutoka kwa uzoefu wako mwenyewe, utakatifu wa Mungu ni upendo Wake tu? Ni upendo wa Mungu tu tunaoelezea kama utakatifu? Huo utakuwa wa upande mmoja sana, siyo? Mbali na upendo wa Mungu, kuna vipengele vingine vya kiini cha Mungu? Je, mmeviona? (Ndiyo. Mungu anachukia tamasha na likizo, mila, na ushirikina; huu pia ni utakatifu wa Mungu.) Mungu ni mtakatifu kwa hivyo Anachukia vitu, inamaanisha hivyo? Katika mizizi ya hayo, ni nini utakatifu wa Mungu? Utakatifu wa Mungu hauna maudhui makubwa, ni kwamba tu Anachukia vitu? Katika akili zenu mnafikiria, “Kwa sababu Mungu anachukia vitu hivi ovu, hivyo mtu anaweza kusema kwamba Mungu ni mtakatifu”? Si huu ni

uvumi hapa? Si hii ni aina ya dhana na hukumu? Ni nini mwiko mkubwa zaidi inapokuja kwa kuelewa kiini cha Mungu? (Ni wakati tunaacha ukweli nyuma kuzungumza kuhusu mafundisho ya kidini.) Huu ndio mwiko mkubwa sana kufanya. Kitu kingine? (Uvumi na ubunifu.) Haya pia ni miiko ya nguvu sana. Mbona uvumi na ubunifu si wa manufaa? Vitu unavyobashiri kuhusu na kufikiria vitu ambavyo kweli unaweza kuona? Ni kiini cha kweli cha Mungu? (La.) Nini tena ni mwiko? Ni mwiko kuhesabu tu kifungu cha maneno yanayosikika kuwa mazuri kueleza kiini cha Mungu? (Ndiyo.) Si huku ni kujigamba na upuuzi? Hukumu na uvumi ni upuuzi, kama tu kuchukua maneno yanayosikika kuwa mazuri. Sifa tupu pia ni upuuzi, siyo? Je, Mungu anafurahia kusikiza watu wakisema upuuzi wa aina hii? (La, hafurahii.) Anahisi kutostareheka kusikia huu upuuzi! Mungu anaongoza na kuokoa kundi la watu, na baada ya kundi hili la watu kusikia maneno Yake hawaelewi Anachomaanisha. Mtu anaweza kuuliza: “Mungu ni mwema?” na wangejibu, “Mwema!” “Mwema vipi?” “Mwema sana sana!” “Mungu anampenda mwanadamu?” “Ndiyo!” “Kiasi gani? Unaweza kuelezea?” “Sana sana zaidi! Ni wa kina zaidi kuliko bahari, wa juu zaidi kuliko anga!” Si huu ni upuuzi? Si huu upuuzi ni sawa na kile mlichotoka kusema kuhusu, “Mungu anachukia tabia potovu ya Shetani, hivyo Mungu ni mtakatifu”? (Ndiyo.) Si kile mlichotoka kusema ni upuuzi? Mengi ya haya mambo ya upuuzi yanayosemwa yanatoka wapi? (Shetani.) Mambo ya upuuzi yanayosemwa kimsingi yanatoka kwa kutowajibika kwa watu na kutomheshimu Mungu. Tunaweza kusema hayo? Hukuwa na uelewa wowote lakini bado uliongea upuuzi, si huku ni kutowajibika? Si ni kutomheshimu Mungu? Umesoma kiasi kidogo cha maarifa, umeelewa kiasi kidogo cha kufikiria, na kiasi kidogo cha mantiki, ambayo umetumia na, zaidi, umefanya hivyo ukimjua Mungu. Unafikiri Mungu anahisi kutostareheka kuyasikia hayo? Mnawezaje kumjua Mungu mkitumia mbinu hizi? Je, si hayo yanasikika kuwa ya kufedhehesha? Kwa hivyo, inapokuja kwa maarifa ya Mungu, mtu lazima awe makini sana; mahali unapojua Mungu, zungumza tu kuhusu hayo. Zungumza kwa uaminifu na kivitendo na usipambe maneno yako na pongezi za kawaida na usitumie sifa isiyostahilika; Mungu haihitaji na kitu kama hiki kinatoka kwa Shetani. Tabia ya Shetani ni ya kiburi na Shetani anapenda kupewa sifa isiyostahilika na kusikia maneno mazuri. Shetani ataridhishwa na kufurahia iwapo watu watataja maneno yote mazuri ambayo wamejifunza na kutumia maneno haya kwa Shetani. Lakini Mungu hahitaji hii; Mungu hahitaji kuvishwa kilemba cha ukoka ama sifa isiyostahilika na Hahitaji kwamba watu wazungumze upuuzi na kumsifu kwa upofu. Mungu anachukizwa sana na hata Hatasikiza sifa ambayo haiko sambamba na ukweli. Hivyo, wakati watu wengine wanamsifu Mungu kwa upofu na kile wanachosema hakilingani na kile kiko katika mioyo yao na wanapofanya viapo kwa upofu na kumwomba ovyo ovyo, Mungu hasikizi hata kidogo. Lazima uwajibike kwa kile unachosema. Ikiwa hujui jambo, sema tu; ikiwa unajua jambo, onyesha hivyo kwa njia ya kitendo. Hivyo, kuhusiana na utakatifu wa Mungu unajumuisha nini hasa na kwa kweli, je, mna ufahamu wa kweli kuhusu hilo?

(Nilipoonyesha uasi, nilipofanya makosa, nilipokea hukumu na kuadibu kwa Mungu, na hapo niliona utakatifu wa Mungu. Na nilipokabiliana na mazingira ambayo hayakukubaliana na matarajio yangu, niliomba kuhusu mambo haya na kutafuta nia za Mungu na Mungu aliponipa nuru na kuniongoza na maneno Yake, niliona utakatifu wa Mungu.) Haya yametoka kwa uzoefu wako mwenyewe. (Kutoka kwa yale ambayo Mungu amezungumza kulihusu, nimeona kile ambacho mwanadamu amekuwa baada ya kupotoshwa na kudhuriwa na Shetani. Hata hivyo, Mungu ametoa yote kutuokoa na kutokana na haya naona utakatifu wa Mungu.) Hii ni njia ya vitendo ya kuzungumza; ni maarifa ya kweli. Je, kuna njia zozote tofauti za kuelewa hili? (Naona uovu wa Shetani kutoka kwa maneno alisema ili kumlaghai Hawa kutenda dhambi na ushawishi wake wa Bwana Yesu. Kutoka kwa maneno ambayo kwayo Mungu aliwaambia Adamu na Hawa kile walichoweza na wasichoweza kula, naona kwamba maneno ya Mungu ni wazi na safi na kwamba ni ya kuaminiwa; kutoka kwa haya naona utakatifu wa Mungu.) Kwa kile mmesikia watu hawa wakisema, mnasema Amina zaidi kwa maneno ya nani? Ushirika wa nani ulikuwa karibu zaidi na ushirika wa mada yetu leo, ya nani ilikuwa ya kweli zaidi? Ushirika wa dada wa mwisho ulikuwa vipi? (Mzuri.) Unasema Amina kwa kile alichosema, ni nini alichosema kilichokuwa sahihi kwa lengo? (Katika maneno ambayo ndugu alizungumza hivi karibuni, nilisikia kwamba neno la Mungu linaeleweka kwa urahisi na ni wazi sana, si kama maneno ya Shetani yasiyo ya moja kwa moja. Niliona utakatifu wa Mungu kwa haya.) Hii ni sehemu ya hayo. Ilikuwa sahihi? (Ndiyo.) Vizuri sana. Naona kwamba mmepata kitu katika shirika hizi mbili za hivi karibuni, lakini lazima nyinyi mwendelee kufanya kazi kwa bidii. Ni lazima mfanye kazi kwa sababu kuelewa kiini cha Mungu ni somo kubwa sana; si kitu ambacho mtu anaweza kuelewa mara moja ama anaweza kuzungumza wazi kwa maneno machache tu.

Kila kipengele cha tabia potovu ya Kishetani ya watu, maarifa, filosofia, fikira na mitazamo ya watu, na vipengele binafsi vinawazuia pakubwa kujua kiini cha Mungu; hivyo mnapozisikia mada hizi, mada zingine zinaweza kuwa mbali kwenu kufikia, mada zingine pengine hamtaelewa, ilhali mada zingine pengine kimsingi hamtalingana nazo na hali halisi. Licha ya hayo, Nimesikia kuhusu uelewa wenu wa utakatifu wa Mungu na Najua kwamba katika mioyo yenu mmeanza kukubali kile Nilichosema na kushiriki kuhusu utakatifu wa Mungu. Najua kwamba katika mioyo yenu hamu yenu ya kuelewa kiini cha utakatifu wa Mungu imeanza kuchipuka. Lakini ni nini kinachonifanya kuwa na furaha zaidi ni kwamba wengine wenu tayari wanaweza kutumia maneno rahisi sana kuelezea maarifa yenu ya utakatifu wa Mungu. Ingawa hiki ni kitu rahisi kusema na Nimekisema awali, katika mioyo ya wengi wenu hii bado haijakubaliwa ama kuweka alama. Hata hivyo, wengine wenu wameweka maneno haya moyoni na ni vizuri kabisa na huu ni mwanzo mzuri sana. Natumai kwamba kwa mada ambazo mnafikiri kuwa za maana sana—ama kwa mada ambazo ziko mbali kwenu kufikia—mtaendelea

kutafakari, na kufanya ushirika zaidi na zaidi. Kwa yale masuala ambayo yako mbali kwenu kufikia kutakuwa na mtu wa kuwapa mwongozo zaidi. Mkishiriki katika ushirika zaidi kuhusu maeneo ambayo mnaweza kufikia sasa, Roho Mtakatifu atafanya kazi Yake na mtakuwa na uelewa mkubwa zaidi. Kuelewa kiini cha Mungu na kujua kiini cha Mungu kuna umuhimu mkubwa zaidi kwa kuingia kwa watu katika maisha. Natumai kwamba hamtapuuza haya ama kuyaona kama mchezo, kwa sababu kumjua Mungu ndio msingi wa imani ya mwanadamu na pia muhimu kwa mwanadamu kufuatilia ukweli na kupata wokovu. Iwapo watu wanamwamini Mungu lakini hawamjui, iwapo wanaishi tu miongoni mwa baadhi ya barua na mafundisho ya kidini, haitawahi kuwezekana wao kufikia wokovu hata kama wanatenda na kuishi kulingana na maana ya juujuu ya ukweli. Hiyo ni kusema, iwapo unamwamini Mungu lakini humjui, basi imani yako ni bure na haina chochote. Unaelewa, sivyo? (Ndiyo, tunaelewa.) Ushirika wetu utaishia hapa kwa leo. (Mshukuru Mungu!)

Januari 4, 2014

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee VI

Utakatifu wa Mungu (III)

Mada tuliyoishiriki wakati uliopita ilikuwa utakatifu wa Mungu. Ni kipengele kipi cha Mungu Mwenyewe kinahusisha utakatifu wa Mungu? Je, kinahusisha kiini cha Mungu? (Ndiyo.) Kwa hivyo ni nini mada inayohusiana na kiini cha Mungu katika ushirika wetu? Je, ni utakatifu wa Mungu? Utakatifu wa Mungu: hiki ni kiini cha kipekee cha Mungu. Ni nini ilikuwa dhamira kuu tuliyoishiriki wakati uliopita? (Utambuzi wa uovu wa Shetani. Yaani, jinsi Shetani anampotosha mwanadamu; anatumia maarifa, sayansi, desturi ya kitamaduni, ushirikina, na mitindo ya kijamii kupotosha mwanadamu.) Hii ndiyo ilikuwa mada kuu tuliyojadili wakati uliopita. Shetani hutumia maarifa, sayansi, ushirikina, desturi ya kitamaduni, na mitindo ya kijamii kumpotosha mwanadamu; hizi ndizo njia ambazo Shetani anampotosha mwanadamu. Hizi ni njia tano kwa jumla. Mnafikiri Shetani anatumia nini zaidi kumpotosha mwanadamu, kitu ambacho kinampotosha kwa kina zaidi? (Desturi ya kitamaduni. Hii ni kwa sababu falsafa za kishetani kama vile mafundisho ya Confucius na Mencius zimetopea sana katika akili zetu.) Baadhi ya ndugu wanafikiri ni desturi za kitamaduni. Mwingine yeyote? (Maarifa. Maarifa hayawezi kuturuhusu kumwabudu Mungu. Yanapinga kuwepo kwa Mungu, na yanapinga kanuni ya Mungu. Yaani, Shetani hutuambia tusome kuanzia umri mdogo, na kwamba ni kupitia tu kusoma na kupata maarifa ndipo siku zetu za baadaye na kudura zetu zinahakikishwa.) Shetani anatumia maarifa kudhibiti siku zako za baadaye na kudura yako, kisha anakuongoza kuendelea kupitia pua lako; hivi ndivyo unavyofikiria Shetani anampotosha mwanadamu kwa kina zaidi. Kwa hivyo wengi wenu wanafikiri Shetani anatumia maarifa kumpotosha mwanadamu kwa kina.

Kuna mengine zaidi? Je, sayansi na mitindo ya kijamii, kwa mfano? Kuna yeyote anayekubaliana na haya? (Ndiyo.) Leo Nitashiriki tena kuhusu njia tano ambazo Shetani anampotosha mwanadamu, na, baada ya Mimi kumaliza, Nitawauliza baadhi ya maswali ili kuona ni katika kipengele kipi hasa Shetani anampotosha mwanadamu kwa kina zaidi.

Kati ya njia tano ambazo Shetani anatumia kumpotosha mwanadamu ni njia tano anavyompotosha mwanadamu, ya kwanza tano tuliyotaja ni maarifa, kwa hivyo wacha kwanza tuchukue maarifa kama mada ya kushiriki. Shetani hutumia maarifa kama chambo. Sikiza kwa makini: Ni aina tu ya chambo. Watu wanavutiwa “kusoma kwa bidii na kuboreka kila siku,” kujihami kwa maarifa, kama silaha, kisha kutumia maarifa kufungua njia ya sayansi; kwa maneno mengine, kadri unapopata maarifa zaidi, ndivyo utakavyoelewa zaidi. Shetani huwaambia watu haya yote. Shetani huwaambia watu kuwa na fikira za juu pia, kwa wakati sawa wanaposoma maarifa, akiwaambia kuwa na matarajio na mawazo. Bila kujua kwa watu, Shetani anasambaza ujumbe mwingi kama huu, na kuwafanya watu kuhisi bila kujua kwamba vitu hivi ni sahihi, ama ni vya manufaa. Bila kujua, watu wanaitembea njia hii, bila kujua wanaongozwa mbele na matarajio na mawazo yao. Hatua kwa hatua, kwa kutojua wanajifunza kutoka kwa maarifa waliyopewa na Shetani njia ambazo watu wakubwa ama maarufu wanafikiria. Wanajifunza pia mambo fulani kutoka kwa matendo ya wengine ambao wanafikiriwa kuwa mashujaa. Shetani anatetea nini kwa mwanadamu katika matendo ya hawa mashujaa? Ni nini anachotaka kuingiza kwa mwanadamu? Mwanadamu lazima awe mzalendo, awe na uadilifu wa kitaifa, na awe shujaa. Ni yapi ambayo mwanadamu anajifunza kutoka kwa baadhi ya hadithi za kihistoria ama kutoka kwa wasifu wa mashujaa? Kuwa na hisia ya uaminifu wa kibinafsi, ama kufanya lolote kwa ajili ya rafiki ya mtu ama kwa rafiki. Miongoni mwa maarifa haya ya Shetani, mwanadamu bila kujua anajifunza mambo mengi hasi. Katikati ya kutojua huku, mbegu zilizotayarishwa kwa ajili yao na Shetani zinapandwa katika akili zao zisizokomaa. Mbegu hizi zinawafanya kuhisi kwamba wanapaswa kuwa watu wakubwa, wanapaswa kuwa maarufu, wanapaswa kuwa mashujaa, kuwa wazalendo, kuwa watu wanaopenda familia zao, ama kuwa watu wanaoweza kufanya chochote kwa ajili ya rafiki na kuwa na hisia za uaminifu wa kibinafsi. Baada ya kushawishiwa na Shetani, bila kujua wanatembea njia ambayo amewatayarishia. Wanapotembea njia hii, wanalazimika kukubali kanuni za Shetani za kuishi. Bila kujua na bila wao kuwa na uelewa kabisa, wanakuwa na kanuni zao za kuishi, wakati hizi si chochote ila kanuni za Shetani ambazo zimeingizwa kwao kwa nguvu. Wakati wa mchakato wa kujifunza, Shetani anawasababisha kukuza malengo yao wenyewe, kuamua malengo yao ya maisha wenyewe, kanuni za kuishi, na mwelekeo wa maisha, wakati huo wote anawaingizia mambo ya Shetani, kwa kutumia hadithi, kwa kutumia wasifu, kwa kutumia mbinu zote zinazowezekana kuwapata watu, kuchukua chambo polepole. Kwa njia hii, katika mkondo wa kujifunza kwao,

wengine wanakuja kupenda fasihi, wengine uchumi, wengine unajimu ama jiografia. Kisha kuna wengine wanaokuja kupenda siasa, wengine wanaopenda fizikia, wengine kemia, na hata wengine wanaopenda teolojia. Haya yote ni sehemu ya maarifa. Katika mioyo yenu, kila mmoja wenu anajua yalivyo na mambo haya, kila mmoja amepatana nayo awali. Kuhusiana na maarifa ya aina hii, yeyote anaweza kuzungumza bila kikomo kuhusu moja yao fulani. Na hivyo ni wazi jinsi maarifa haya yameingia kwa kina katika akili ya mwanadamu, pia inaonyesha nafasi iliyochukuliwa na maarifa haya katika akili ya mwanadamu na jinsi yalivyo na athari ya kina kwa mwanadamu. Punde tu mtu anapenda sehemu ya maarifa, wakati katika moyo wake mtu amependa kwa dhati mojawapo, basi bila kujua anaendeleza mawazo: Watu wengine wanataka kuwa watunzi, wengine wanataka kuwa waandishi, wengine wanataka kuwa na kazi kutokana na siasa, na wengine wanataka kushiriki katika uchumi na kuwa wanabiashara. Kisha kuna kundi la watu ambao wanataka kuwa mashujaa, kuwa wakubwa ama maarufu. Bila kujali mtu anataka kuwa mtu wa aina gani, lengo lake ni kuchukua mbinu hii ya kujifunza maarifa na kuitumia kwa ajili yake, kufikia matamania yake, mawazo yake mwenyewe. Haijalishi inasikika kuwa nzuri namna gani—anataka kufikia ndoto yake, asiishi katika maisha haya bure, ama anataka kushiriki katika kazi—anakuza haya mawazo na matarajio ya juu lakini, kimsingi, yote ni ya nini? Je, mmeyafikiria haya awali? Mbona Shetani anataka kufanya hivi? Madhumuni ya Shetani ni yapi katika kuyaweka mambo haya kwa mwanadamu? Mioyo yenu lazima ielewe vizuri swali hili.

Sasa wacha tuzungumze kuhusu jinsi Shetani hutumia maarifa kumpotosha mwanadamu. Kwanza, tunapaswa kuwa na ufahamu wazi wa haya mambo: Kwa maarifa, ni kipi ambacho Shetani Anataka kumpa mwanadamu? Anataka kumfanyia nini mwanadamu kwa kutumia maarifa? Kumwongoza mwanadamu kufuata njia ya aina gani? (Kumpinga Mungu.) Bila shaka ni kumpinga Mungu. Hii ni matokeo unayoweza kuyaona kutoka kwa watu kupata maarifa—kumpinga Mungu. Hivyo ni nini malengo husuda ya Shetani? Hujayaelewa, sio? Katika mchakato wa mwanadamu kujifunza maarifa, Shetani atatumia mbinu zozote, iwe kufafanua hadithi, akimpa tu kipande kimoja cha maarifa, au kumruhusu aridhishe tamaa zake au aridhishe mawazo. Shetani anataka kukuongoza katika njia gani? Watu wanafikiri kwamba hakuna chochote kibaya na kujifunza maarifa, kwamba ni mkondo wa kiasili. Kuisema bila kutia chumvi, kukuza mawazo ya juu ama kuwa na matarajio ni kuwa na hamu ya kupata, na hii inapaswa kuwa njia sawa katika maisha. Iwapo watu wanaweza kufanikisha mawazo yao wenyewe, ama kuwa na kazi maishani mwao—je, si ni adhimu zaidi kuishi namna hii? Sio tu kuheshimu babu za mtu kwa njia hiyo bali pia ikiwezekana kuacha alama yako katika historia—hili si jambo zuri? Hili ni jambo zuri katika macho ya watu wa kidunia na kwao linapaswa kuwa la kufaa na njema. Je, Shetani, hata hivyo, na malengo yake husuda, anawapeleka tu watu kwa njia ya aina hii na kisha kuamua amemaliza? Bila shaka la. Kwa kweli, haijalishi jinsi yalivyo

juu mawazo ya mwanadamu, haijalishi matamano ya mwanadamu ni ya uhalisi jinsi gani ama jinsi yote yanaweza kuwa ya kufaa, yote ambayo mwanadamu anataka kufikia, yote ambayo mwanadamu anatafuta yameunganishwa bila kuchangulika na maneno mawili. Haya maneno mawili ni muhimu sana kwa maisha ya kila mtu, na haya ni mambo ambayo Shetani ananua kuingiza ndani ya mwanadamu. Maneno haya mawili ni yapi? Ni “umaarufu” na “faida”: Shetani anatumia njia ya hila sana, njia ambayo iko pamoja sana na dhana za watu; si aina ya njia kali. Katikati ya kutoelewa, watu wanakuja kukubali njia ya Shetani ya kuishi, kanuni zake za kuishi, kuanzisha malengo ya maisha na mwelekeo wao katika maisha, na kwa kufanya hivyo wanakuja pia bila kujua kuwa na mawazo katika maisha. Haijalishi mawazo haya yanaonekana kusikika kuwa ya juu kiasi gani katika maisha, ni kisingizio tu ambacho kinahusiana kwa kutochangulika kwa umaarufu na faida. Mtu yeyote aliye mkubwa ama maarufu, watu wote kwa hakika, chochote wanachofuata maishani kinahusiana tu na haya maneno mawili: “umaarufu” na “faida.” Watu hufikiri kwamba punde tu wanapata umaarufu na faida, wanaweza basi kuyatumia kwa faida yao kufurahia hadhi ya juu na utajiri mwingi, na kufurahia maisha. Baada ya wao kuwa na umaarufu na faida, wanaweza basi kuyatumia kwa faida yao katika kutafuta kwao raha na kufurahia kwao kwa fidhuli mwili. Watu kwa hiari, lakini bila kujua, wanachukua miili na akili zao na vyote walivyonavyo, siku zao za baadaye, na kudura zao na kuzikabidhi zote kwa Shetani ili kupata umaarufu na faida wanayotaka. Watu kweli hufanya hivi kamwe bila kusita kwa muda, kamwe bila kujua haja ya kupata tena yote. Je, watu bado wanaweza kujidhibiti baada ya wao kumkimbilia Shetani na kuwa mwaminifu kwake kwa njia hii? Bila shaka, la. Wanadhhibitiwa na Shetani kikamilifu na kabisa. Pia kikamilifu na kabisa wamezama katika bwawa na hawawezi kujinusuru. Baada ya mtu kukwama katika umaarufu na faida, hatafuti tena kile kilichong’aa, kile chenye haki ama yale mambo ambayo ni mazuri na mema. Hii ni kwa sababu nguvu za ushawishi ambazo umaarufu na faida yanayo juu ya watu ni kubwa mno, na vinakuwa vitu vya watu kutafuta katika maisha yao yote na pia milele bila kikomo. Hili si ukweli? Watu wengine watasema kwamba kujifunza maarifa si chochote zaidi ya kusoma vitabu ama kujifunza mambo kadhaa ambayo hawajui tayari, ili wasiwe nyuma ya nyakati ama wasiwachwe nyuma na dunia. Maarifa yanafunzwa tu ili waweze kuweka chakula mezani, kwa sababu ya siku zao za baadaye ama kwa sababu ya mahitaji ya kimsingi. Kuna mtu yeyote ambaye atastahimili mwongo wa kusoma kwa bidii kwa mahitaji ya kimsingi tu, ili kutatua swala la chakula tu? Hakuna watu kama hawa. Kwa hivyo ni nini anatesekea matatizo haya na kutesekea miaka hii yote? Ni kwa sababu ya umaarufu na faida: Umaarufu na faida yanamngoja mbele, yanamwita, na anaamini tu kwa kupitia bidii yake mwenyewe, matatizo na mapambano ndiyo anaweza kufuata ile njia na hivyo kupata umaarufu na faida. Lazima ateseke matatizo haya kwa sababu ya njia yake ya siku za baadaye, kwa sababu ya raha yake ya siku za baadaye na kwa sababu ya maisha bora. Mnaweza kuniambia—haya maarifa kwa hakika ni nini? Si kanuni za kuishi ziliyoingizwa kwa

watu na Shetani, zilizofundishwa kwao na Shetani katika kujifunza kwao maarifa? Je, si mawazo juu ya maisha yaliyoingizwa kwa mwanadamu na Shetani? Chukua, kwa mfano, mawazo ya watu wakubwa, uadilifu wa watu maarufu ama roho jasiri ya watu mashujaa, ama chukua uungwana na wema wa nguli na wenye panga katika riwaya za kareti. (Ndiyo, ni kweli.) Mawazo haya yanashawishi kizazi kimoja baada ya kingine, na watu wa kila kizazi wanaletwa kuyakubali mawazo haya, kuishi kwa sababu ya mawazo haya na kuyafuata bila kikomo. Hii ndiyo njia, mbinu, ambayo Shetani anatumia maarifa kumpotosha mwanadamu. Kwa hivyo baada ya Shetani kuwaongoza watu kwa njia hii, inawezekana wao kumwabudu Mungu? Je, maarifa na fikira zilizolingizwa kwa mwanadamu na Shetani zina yoyote kuhusu kumwabudu Mungu? Zina fikira yoyote ya ukweli? Je, zina uhalisi wowote wa kumcha Mungu na kuepuka uovu. (La, hazina.) Mnaonekana kuongea bila uhakika kidogo, lakini haijalishi. Alimradi mtambue kwamba “umaarufu” na “faida” ni maneno mawili muhimu ambayo Shetani hutumia kuwashawishi watu kuingia njia ya uovu, basi hilo limetosha.

Acha turejeele tena kwa ufupi: Shetani hutumia nini kuendelea kumfungia mwanadamu na kumdhibiti? (Umaarufu na faida.) Kwa hivyo Shetani hutumia umaarufu na faida kudhibiti fikira za mwanadamu hadi anachofikiria tu ni umaarufu na faida. Wanapambana kwa sababu ya umaarufu na faida, wanateseka matatizo kwa sababu ya umaarufu na faida, wanastahimili udhalilishaji kwa sababu ya umaarufu na faida, wanatoa kila kitu walichonacho kwa sababu ya umaarufu na faida, na watafanya maoni au uamuzi wowote kwa ajili ya umaarufu na faida. Kwa njia hii, Shetani humfunga mwanadamu kwa pingu zisizoonekana. Pingu hizi zinabebwa na watu, na hawana nguvu ama ujasiri wa kuzirusha mbali. Kwa hivyo, bila kujua, watu huvumilia pingu hizi na kutembea kwenda mbele kwa ugumu mkubwa. Kwa ajili ya umaarufu huu na faida hii, binadamu humwepuka Mungu na kumsaliti, na wanazidi kuwa waovu zaidi na zaidi. Kwa njia hii, hivyo kizazi kimoja baada ya kingine kinaharibiwa katika umaarufu na faida ya Shetani. Tukiangalia sasa vitendo vya Shetani, nia zake husuda ni za kuchukiza? Pengine leo bado hamwezi kuona kupitia nia husuda za Shetani kwa sababu mnafikiri hakuna maisha bila umaarufu na faida. Mnafikri kwamba, iwapo watu wataacha umaarufu na faida nyuma, basi hawataweza tena kuona njia mbele, hawataweza tena kuona malengo yao, siku zao za baadaye zawa giza, zilizofifia na za ghamu. Lakini, polepole, nyote siku moja mtatambua kwamba umaarufu na faida ni pingu za ajabu ambazo Shetani hutumia kumfunga mwanadamu. Hadi ile siku utakuja kutambua hili, utapinga kabisa udhibiti wa Shetani na utapinga kabisa pingu anazoleta Shetani kukufunga. Wakati utakapofika wa wewe kutaka kutupilia mbali vitu vyote ambavyo Shetani ameingiza ndani yako, utakuwa basi umejiondoa kwa Shetani na pia utachukia kwa kweli vyote ambavyo Shetani amekuletea. Hapo tu ndipo utakuwa na upendo na shauku ya kweli kwa Mungu.

Tumetoka tu kuongea kuhusu jinsi Shetani hutumia maarifa kumpotosha mwanadamu, basi kinachofuata wacha tushiriki kuhusu jinsi Shetani hutumia sayansi kumpotosha mwanadamu. Kwanza, Shetani hutumia jina la sayansi kuridhisha hamu ya mwanadamu kutafiti sayansi na kuchunguza siri. Kwa jina la sayansi, Shetani huridhisha haja ya mwili na mahitaji ya mwanadamu kuendelea kuinua ubora wao wa maisha. Shetani hivyo, katika jina hili, hutumia njia ya sayansi kumpotosha mwanadamu. Je, ni kufikiria tu kwa mwanadamu ama akili za mwanadamu ambazo Shetani anapotosha kwa kutumia njia hii ya sayansi? Miongoni mwa watu, matukio na mambo katika mazingira yetu ambayo tunaweza kuona na ambayo tunakutana nayo, ni yapi mengine ambayo Shetani anatumia sayansi kupotosha? (Mazingira ya kiasili.) Mko sahihi. Inaonekana kwamba mmedhuriwa sana na hili, na pia mmeathirika sana na yeye. Mbali na kutumia matokeo yote ya utafiti na mahitimisho mbalimbali ya sayansi kumdanganya mwanadamu, Shetani pia hutumia sayansi kama mbinu ya kutekeleza maangamizi na unyonyaji tele wa mazingira ya kuishi aliyopewa mwanadamu na Mungu. Anafanya hivi chini ya kisingizio kwamba iwapo mwanadamu anatekeleza utafiti wa kisayansi, mazingira ya kuishi ya mwanadamu yatakuwa bora na bora zaidi na viwango vya kuishi vya mwanadamu daima vitaboreka, na zaidi ya hayo kwamba maendeleo ya kisayansi yanafanywa ili kuhudumia mahitaji ya mwili ya mwanadamu yanayozidi kila siku na haja yao ya kuendelea kupandisha ubora wao wa maisha. Huu ni msingi wa kidhahania wa maendeleo ya Shetani ya sayansi. Hata hivyo, sayansi imemletea binadamu nini? Mazingira yetu ya karibu kabisa yana nini? Si hewa ambayo binadamu hupumua imechafuliwa? Maji tunayoyanywa kweli bado ni safi? (La.) Chakula tunachokula, ni cha kiasili? Kingi kinapandwa kutumia mbolea na kinakuzwa kutumia vinasaba, na pia kuna mabadiliko yanayozalishwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za sayansi. Hata mboga na matunda tunayoyala sio ya kiasili tena. Si rahisi sasa kwa watu kupata yai la asili kula. Na mayai hayaonji yalivyokuwa yakionja awali, baada ya kusindikwa na inayoitwa sayansi na Shetani. Kwa kuangalia taswira kubwa, anga nzima imeharibika na kuchafuliwa; milima, maziwa, misitu, mito, bahari, na kila kitu juu na chini ya ardhi vyote vimeharibiwa na inayoitwa mafanikio ya kisayansi. Kwa maneno mengine, mazingira yote ya kiikolojia, mazingira ya kuishi yaliyopewa mwanadamu na Mungu yameangamizwa na kuharibiwa na inayodaiwa kuwa sayansi. Ingawa kuna watu wengi waliopata walichotarajia katika suala la ubora wa maisha wanaotafuta, kuridhisha tamaa na miili yao, mazingira ambayo mwanadamu anaishi kimsingi yameharibiwa na kuangamizwa na “mafanikio” mbalimbali yaliyoletwa na sayansi. Sasa, hatuna tena haki ya kupumua pumzi moja ya hewa safi. Hii ni huzuni ya mwanadamu? Bado kuna furaha yoyote ya kuzungumzia kwa mwanadamu kuishi katika nafasi hii ya kuishi? Mwanadamu anaishi katika nafasi hii ya kuishi na, kutoka mwanzoni, haya mazingira ya kuishi yaliumbwa na Mungu kwa ajili ya mwanadamu. Maji ambayo watu hunywa, hewa ambayo watu hupumua, chakula ambacho watu hula, mimea, miti, na bahari—haya mazingira ya kuishi yote yalipewa

mwanadamu na Mungu; ni asili, na hutekeleza kulingana na amri asili iliyotolewa na Mungu. Kama hakungekuwa na sayansi, watu wangukuwa na furaha na wangufurahia kila kitu kikiwa cha asili kabisa kulingana na njia ya Mungu na kulingana na kile Mungu amewapa wafurahie. Sasa, hata hivyo, haya yote yameangamizwa na kuharibiwa na Shetani; nafasi ya kimsingi ya kuishi ya mwanadamu haipo tena katika hali yake asili zaidi. Lakini hakuna anayeweza kutambua kilichosababisha matokeo ya aina hii ama jinsi haya yalikuja kuwa, na zaidi ya hapo hata watu zaidi wanaelewa na kukaribia sayansi kwa kutumia mawazo waliyoingiziwa na Shetani Je, hii si ya kuchukiza sana na ya kusikitisha? Kwa kuwa Shetani sasa amechukua nafasi ambamo wanadamu wapo na mazingira yao ya kuishi na kuwapotosha kuwa katika hali hii, na kwa kuwa wanadamu wanaendelea kwa njia hii, kuna haja yoyote ya mkono wa Mungu kuwaangamiza wanadamu hawa duniani? Iwapo wanadamu watazidi kuendelea kwa njia hii, watachukua mwelekeo upi? (Wataangamizwa.) Wataangamizwa kwa njia gani? Zaidi ya mwanadamu kutafuta kwa tamaa umaarufu na faida, daima anaendelea kutekeleza uchunguzi wa sayansi na utafiti wa kina, kisha bila kikomo huridhisha mahitaji yake ya mwili na tamaa; yapi tena ni matokeo ya mwanadamu? Kwanza kabisa hakuna tena usawa wa ikolojia na, pamoja na hili, miili ya wanadamu yote imetiwa doa na kuharibiwa na mazingira ya hali hii, na magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na mapigo kusambaa kila mahali. Hii ni hali ambayo mwanadamu sasa hawezi kudhibiti, sivyo? Sasa kwa sababu mnaelewa hili, iwapo wanadamu hawamfuati Mungu, lakini daima wanamfuata Shetani kwa njia hii—kutumia maarifa daima kujitajirisha, kutumia sayansi kuchunguza bila kikomo siku za baadaye za maisha ya binadamu, kutumia mbinu ya aina hii kuendelea kuishi—mnaweza kutambua mwisho wa asili wa wanadamu utakuwa vipi? (Maangamizi.) Itakuwa uharibifu: kukaribia uharibifu hatua moja kwa wakati. Kukaribia uharibifu kwa hatua moja kwa wakati! Inaonekana sasa kama sayansi ni aina ya ushombwe ambao Shetani amemwandalia mwanadamu, ili wakati mnapojaribu kupambanua mambo mnafanya hivyo katika hali ya ukungu; haijalishi mnaangalia kwa ugumu aje, hamwezi kuona mambo kwa wazi, na haijalishi mnajaribu sana vipi, hamwezi kuyatambua. Shetani, hata hivyo, bado anatumia jina la sayansi kuzidisha hamu yako na kukuongoza kwa pua, mguu mmoja mbele ya mwingine, kuelekea shimo na kuelekea kifo. Sivyo? (Ndiyo.) Hii ndiyo njia ya pili.

Njia ya tatu ni jinsi Shetani hutumia desturi ya kitamaduni kumpotosha mwanadamu. Kuna usawa mwingi kati ya desturi ya kitamaduni na ushirikina, ni tu kuwa desturi ya kitamaduni ina hadithi fulani, vidokezo, na vyanzo fulani. Shetani ametunga na kuunda ngano ama hadithi nyingi katika vitabu vya historia, na kuacha watu na hisia za kina za desturi ya kitamaduni ama watu wa kishirikina. Chukua kwa mfano Watu Wanane Wasiokufa Wanaovuka Bahari, Safari ya kwenda Magharibi, Mfalme Mkuu Jade, Nezha Anamshinda Joka Mfalme, na Uchunguzi wa

Miungu, zote za Uchina. Haya hayajakita mizizi katika akili za mwanadamu? Hata iwapo baadhi yenu hawajui maelezo yote, bado mnajua hadithi za jumla, na yaliyomo kwa jumla ndiyo yanayokwama katika moyo wako na yanakwama katika akili yako, na huwezi kuyasahau. Hizi ni dhana au hadithi ambazo Shetani alimwandalia mwanadamu kitambo sana, na ambazo zimesambazwa katika nyakati tofauti. Haya mambo yanadhuru moja kwa moja na kumomonyoa nafsi za watu na kuweka watu chini ya fingo moja baada ya jingine. Hiyo ni kusema kwamba baada ya wewe kukubali aina hii ya desturi ya kitamaduni, hadithi ama vitu vya ushirikina, mara tu mambo haya yanawekwa kwa akili yako, na mara tu yanakwama katika moyo wako, basi ni kama umeduwazwa—unakamatwa na kushawishika na hizi mitego ya kitamaduni, haya mawazo na hadithi za kitamaduni. Yanashawishi maisha yako, mtazamo wako wa maisha na pia yanashawishi maoni yako ya mambo. Hata zaidi yanashawishi ufuataji wako wa njia sahihi ya maisha: Hii bila shaka ni apizo. Unajaribu lakini huwezi kuyatupilia mbali; unayakatakata lakini huwezi kuyakata chini; unayapiga lakini huwezi kuyapiga chini. Zaidi ya hayo, baada ya mwanadamu bila kujua kuwekwa chini ya aina hii ya apizo, bila kujua, anaanza kumwabudu Shetani, kukuza taswira ya Shetani katika moyo wake. Kwa maneno mengine, anamweka Shetani kama sanamu, kifaa cha yeye kuabudu na kutazamia, hata kwenda mbali kiasi cha kumchukulia kama Mungu. Bila kujua, mambo haya yako katika mioyo ya watu yakidhibiti maneno na matendo yao. Aidha, kwanza unachukulia hadithi na hekaya hizi kuwa uongo, na kisha bila kujua unakubali kuwepo kwa hadithi hizi, kuzitengenezea sanamu halisi na kuzibadili kuwa mambo halisi yaliyopo. Katika kutojua, unapokea haya mawazo bila kufahamu na kuwepo kwa vitu hivi. Pia unapokea bila kufahamu mashetani, Shetani na sanamu ndani ya nyumba yako na ndani ya moyo wako—hii bila shaka ni apizo. Je, mnahisi sawa? (Ndiyo.) Kuna yeyote miongoni mwenu ambao wamechoma ubani na kuabudu Budha? (Ndiyo.) Kwa hivyo madhumuni ya kuchoma ubani na kumwabudu Budha yalikuwa yapi? (Kuombea amani.) Kwa kuifikiria sasa, ni ujinga kuombea amani kutoka kwa Shetani? Shetani analeta amani? (La.) Je, mlikuwa wajinga hapo nyuma? Namna ya aina hiyo ni ya upuuzi, jinga na nyofu, siyo? Shetani anafikiria tu jinsi ya kukupotosha na hawezi kukupa amani; anaweza tu kukupa nafasi ya kupumua ya muda mfupi. Lakini lazima uchukue kiapo na ukivunja ahadi yako ama ukivunja kiapo ulichofanya, basi utaona jinsi anavyokuadhibu. Kwa kukufanya uchukue kiapo, kwa kweli anataka kukudhibiti. Wakati mlipoombea amani, mlipata amani? (La.) Hamkupata amani, lakini kinyume na hayo alileta bahati mbaya, majanga yasiyoisha kweli bahari isiyo na mipaka ya uchungu. Amani haiko miongoni mwa miliki ya Shetani, na hili ni ukweli. Haya ndiyo matokeo kwa wanadamu ya ushirikina wa kikabila na desturi ya kitamaduni.

Suala la mwisho ni jinsi Shetani kutumia kwa manufaa yake mitindo ya kijamii kumpotosha mwanadamu. Hii mitindo ya kijamii ina mambo mengi. Watu wengine husema: “Je, inamaanisha

mitindo ya karibuni, vipodozi, kutengeneza nywele na chakula cha kidomo?” Je, ni kuhusu mambo haya? Hii ni sehemu ya mitindo, lakini hatutaki kuzungumzia haya hapa. Tunataka tu kuzungumza kuhusu mawazo ambayo mitindo ya kijamii inaleta kwa watu, jinsi inasababisha watu kutenda duniani, malengo ya maisha na mtazamo ambao inaleta kwa watu. Hii ni muhimu sana; inaweza kudhibiti na kushawishi hali ya akili ya mwanadamu. Moja baada ya nyingine, hii mitindo yote inabeba ushawishi mwovu unaoendelea kumpotosha mwanadamu, kumfanya kuendelea kupoteza dhamiri, ubinadamu na mantiki, na unaoshukisha maadili yao na ubora wao wa tabia zaidi na zaidi, hadi kwa kiwango ambamo tunaweza hata kusema wengi wa watu sasa hawana uadilifu, hawana ubinadamu, wala hawana dhamiri yoyote, wala akili yoyote. Hivyo mitindo hii ni ipi? Huwezi kuona mitindo hii kwa macho. Wakati upepo wa mwenendo unavuma, pengine ni idadi ndogo ya watu tu watakuwa waanzisha mitindo. Wanaanza kwa kufanya jambo la aina hii, kukubali wazo la aina hii ama mtazamo wa aina hii. Wengi wa watu, hata hivyo, katikati ya kutojua kwao, bado watazidi kuambukizwa, kufanywa wenyeji na kuvutia na aina hii ya mwenendo, hadi wote bila kujua na bila kujitolea wanamkubali, na wote wanazama na kudhibitiwa na yeye. Moja baada ya nyingine, mitindo ya aina hii inawafanya watu ambao si wa mwili na akili timamu, wasiojua ukweli, na hawawezi kutofautisha kati ya vitu vyema na hasi, mitindoinawafanya kukubali mitindokwa furaha vilevile mtazamo wa maisha, na maadili yatokayo kwa Shetani. Wanakubali anachowaambia Shetani kuhusu jinsi ya kukaribia maisha na jinsi ya kuishi ambayo Shetani “amewapa.” Na hawana nguvu, wala uwezo, wala ufahamu wa kupinga. Kwa hivyo, hii mitindo hasa ni nini? Nimechukua mfano rahisi ambao mnaweza kuja kuelewa. Kwa mfano, watu wa kale waliendesha biashara zao kwa njia ambayo haikudanganya wazee wala vijana, na ambayo iliua bidhaa kwa bei sawa bila kujali aliyekuwa akinunua. Je, dokezo la dhamiri na ubinadamu haliwasilishwi hapa? Wakati watu walitumia aina hii ya imani walipokuwa wakifanya biashara zao, inaonyesha kwamba bado walikuwa na baadhi ya dhamiri, baadhi ya ubinadamu wakati huo. Lakini na mahitaji ya mwanadamu ya kiasi kinachopanda daima cha pesa, watu bila kujua walikuja kupenda pesa, hupenda faida na hupenda raha zaidi na zaidi. Kwa hivyo watu walikuja kuona pesa kuwa muhimu zaidi? Wakati watu wanaona pesa kuwa muhimu zaidi, bila kujua wanapuuza sifa, umashuhuri wao, ufahari, na uadilifu wao, sivyo? Unapojihusisha katika biashara, unaona wengine wakitumia njia mbalimbali kuibia watu na kuwa tajiri. Ingawa pesa iliyopatwa ni faida iliyopatwa vibaya, wanakuwa tajiri zaidi na zaidi. Wanajihusisha na biashara sawa na wewe, lakini familia yao yote inafurahia maisha kukuliko, na unahisi vibaya, ukisema: “Mbona siwezi kufanya hivyo? Mbona siwezi kupata kama wapatavyo? Ni lazima nifikirie njia ya kupata pesa zaidi, kufanya biashara yangu kufanikiwa.” Kisha unajitahidi kufikiria jinsi ya kuchuma pesa nyingi. Kulingana na mbinu ya kawaida ya kutengeneza pesa, kutodanganya wazee wala vijana na kuuza vitu kwa bei sawa kwa wote, pesa unayotengeneza ni kwa dhamiri nzuri, lakini haiwezi kukufanya kuwa tajiri haraka.

Hata hivyo, chini ya tamaa ya kutengeneza faida, kufikiria kwako kunapitia mabadiliko taratibu. Katika mabadiliko haya, kanuni zako za tabia pia zinaanza kubadilika. Wakati unamdanganya mtu kwa mara ya kwanza, una mashaka, ukisema “Hii ni mara ya mwisho namdanganya mtu na sitafanya hivyo tena. Siwezi kudanganya watu. Kudanganya watu kutapata tu adhabu na kutaleta majanga kwangu!” Unapomdanganya mtu kwa mara ya kwanza, moyo wako una aibu kiasi; hii ndiyo kazi ya dhamiri ya mwanadamu—kuwa na aibu na kukushutumu, ili ihisi kuwa siyo asili wakati unamdanganya mtu. Lakini baada ya wewe kufanikiwa kumdanganya mtu unaona kwamba sasa una pesa zaidi kuliko awali, na unafikiria mbinu hii inaweza kuwa ya manufaa sana kwako. Licha ya maumivu madogo ndani ya moyo wako, bado unahisi kujipongeza kwa mafanikio yako, na unahisi kuridhishwa kidogo na wewe mwenyewe. Kwa mara ya kwanza, unakubali tabia yako mwenyewe na unakubali uwongo wako mwenyewe. Baadaye, wakati mwanadamu amechafuliwa na kudanganywa huku, ni sawa na mtu ambaye anahusika na kamari na kisha anakuwa mchezaji kamari. Katika kutoelewa, anapenda tabia yake ya kudanganya na anaikubali. Katika hali yako ya kutoelewa, unakubali udanganyifu. Katika hali yako ya kutoelewa unachukua udanganyifu kuwa tabia halali ya kibiashara, na unachukua kudanganya kuwa mbinu ya manufaa zaidi ya kusalimika kwako na riziki yako; unafikiria kwamba kwa kufanya hivi anaweza kutengeneza mali nyingi haraka. Huu ni mchakato: Mwanzoni mwa mchakato huu watu hawawezi kukubali tabia ya aina hii, wanadharau tabia hii na njia hii ya kufanya mambo, kisha wanajaribu tabia hii wao wenyewe, na kuijaribu kwa njia yao wenyewe, na kisha mioyo yao inanza kubadilika polepole. Kwa hivyo mabadiliko haya ni yapi? Ni kukubali na kukiri mwenendo huu, kukiri na kukubali wazo hili lililoingizwa kwako na mwenendo wa jamii. Kwa kutojua, unahisi kwamba usipodanganya watu katika kufanya biashara nao, unahisi umebaki nyuma sana; usipodanganya watu unahisi kuwa umepoteza kitu. Bila kujua, kudanganya huku kunakuwa nafsi yako, tegemeo kuu kwako, na kunakuwa aina ya tabia ya lazima ambayo ni kanunimaishani mwako. Baada ya mwanadamu kukubali tabia hii na kufikiria huku, je, moyo wa mwanadamu unapitia mabadiliko? Moyo wako umebadilika, basi uadilifu wako umebadilika? Ubinadamu wako umebadilika? Dhamiri yako imebadilika? (Ndiyo.) Uwepo wote wa mwanadamu unapitia mabadiliko bora, kutoka kwa mioyo yao hadi kwa mawazo yao, hadi kwa kiwango ambapo wanabadilika kutoka ndani hadi nje. Mabadiliko haya yanakuweka mbali na mbali zaidi kutoka kwa Mungu, na unapatana zaidi na zaidi na Shetani, unakuwa sawa zaidi na zaidi na yeye.

Unapotazama mitindo hii ya kijamii, je, unaweza kusema kuwa ina ushawishi mkubwa kwa watu? Je, ina athari inayodhuru kwa kina kwa watu? (Ndiyo.) Mitindo hii ina athari ya kudhuru kwa kina kwa watu. Shetani hutumia moja ya mitindo hii ya kijamii baada ya nyingine kupotosha nini ya mwanadamu? (Dhamiri, akili, ubinadamu, maadili na mtazamo wa maisha.)

Je, inasababisha kuzorota polepole ndani ya watu? Shetani hutumia hii mitindo ya kijamii kuvuta watu hatua moja baada ya nyingine hadi katika kiota cha mashetani, ili watu walionaswa katika mitindo ya kijamii bila kujua wanatetea pesa na tamaa za mwili, na pia kutetea uovu na ukatili. Punde mambo haya yameingia moyoni mwa mwanadamu, ni nini basi mwanadamu anakuwa? Mwanadamu anakuwa ibilisi Shetani! Hii ni kwa sababu ya mwelekeo kisaikolojia upi katika moyo wa mwanadamu? Ni kipi ambacho mwanadamu anatetea? Mwanadamu huanza kupenda uovu na ukatili. Hawapendi uzuri ama wema, wala hata amani. Watu hawako radhi kuishi maisha rahisi ya ubinadamu wa kawaida, lakini badala yake wanataka kufurahia hadhi ya juu na utajiri mkubwa, kufurahia raha za mwili, na kutumia juhudi zote kuridhisha miili yao, bila vizuizi, hakuna vifungo vya kuwashikilia nyuma, kwa maneno mengine kufanya chochote wanachotaka. Hivyo wakati mwanadamu ametumbukizwa katika mitindo ya aina hii, maarifa ambayo mmefunzwa yanaweza kuwasaidia kuwa huru? Je, desturi ya kitamaduni na ushirikina mnayojua yanaweza kuwasaidia kutupilia mbali hii hatari ya kutisha? Je, maadili ya desturi na sherehe za desturi ambazo mwanadamu huelewa zinaweza kumsaidia kujizuia? Chukua Fasihi Bora ya Herufi Tatu, kwa mfano. Inaweza kusaidia watu kutoa miguu yao katika mchanga unaomeza wa mitindo hii? (La, haiwezi.) Kwa njia hii, mwanadamu anakuwa mwovu zaidi na zaidi, mwenye kiburi, mwenye kushusha hadhi, mwenye ubinafsi, na mwenye kijicho. Hakuna tena upendo kati ya watu, hakuna tena upendo wowote kati ya wanafamilia, hakuna tena uelewa wowote miongoni mwa jamaa na marafiki; mahusiano ya binadamu yamejawa ukatili. Kila mtu anataka kutumia mbinu katili kuishi miongoni mwa wanadamu wenzake; wanakamata riziki zao kwa kutumia ukatili; wanashinda vyeo vyao na kupata faida zao wenyewe kwa kutumia ukatili na wanafanya chochote watakacho kwa kutumia njia mbovu na katili. Si ubinadamu huu unatisha? (Ndiyo.) Baada ya kusikia vitu hivi vyotenimetoka kuongea kuhusu, hamfikiri kwamba inatisha kuishi katika mazingira haya, katika ulimwengu huu, na miongoni mwa aina hii ya umati, ambayo Shetani hupitia kupotosha watu? (Ndiyo.) Kwa hivyo mmewahi kujihisi kuwa wenye kusikitisha? Lazima mnaihisi kiasi sasa, siyo? (Ndiyo.) Kwa kusikiza sauti zenu, inaonekana kana kwamba mnafikiria “Shetani hutumia njia nyingi mbalimbali kumpotosha mwanadamu. Anakamata kila fursa na yupo kila mahali tunageukia. Mwanadamu bado anaweza kuokolewa?” Mwanadamu bado anaweza kuokolewa? Wanadamu wanaweza kujiokoa? (La.) Je, Mfalme Mkuu wa Jade anaweza kumwokoa mwanadamu? Je, Confucius anaweza kumwokoa mwanadamu? Je, Guanyin Bodhisattva anaweza kumwokoa mwanadamu? (La.) Kwa hivyo ni nani anayeweza kumwokoa mwanadamu? (Mungu.) Watu wengine, hata hivyo, wataibua katika mioyo yao maswali kama: “Shetani anatudhuru kwa kiasi kikubwa sana, kwa hasira sana basi hatuna matumaini ya kuishi, wala imani katika kuishi. Sote tunaishi miongoni mwa upotovu na kila mtu anampinga Mungu hata hivyo, na sasa mioyo yetu imezama chini kadri iwezavyo. Kwa hivyo wakati Shetani anatupotosha, Mungu yuko wapi? Mungu anafanya nini? Chochote Mungu

anatufanyia kamwe hatukihisi!” Watu wengine bila kuepukika wanahisi kuhuzunika na bila kuepukika wanahisi kuvunjika moyo kiasi, siyo? Kwenu, hisia hii ni ya kina sana kwa sababu vyote ambavyo Nimekuwa nikisema vimekuwa kuwafanya watu kuja kuelewa polepole, kuhisi zaidi na zaidi kwamba hawana matumaini, kuhisi zaidi na zaidi kwamba wameachwa na Mungu. Lakini usijali. Mada yetu ya kushiriki leo, “uovu wa Shetani,” siyo dhamira yetu ya kweli. Kuongea kuhusu kiini cha utakatifu wa Mungu, hata hivyo, lazima kwanza tuingee kuhusu jinsi Shetani anampotosha mwanadamu na uovu wa Shetani ili kuifanya kuwa wazi zaidi kwa watu mwanadamu sasa yuko katika hali ya aina gani. Lengo moja la kuongea juu ya hili ni kuruhusu watu kujua uovu wa Shetani, ilhali jingine ni kuwaruhusu watu kuelewa kwa kina zaidi utakatifu ni nini.

Je, haya mambo ambayo Nimeongea kuhusu hivi karibuni ni ya kina zaidi kuliko ya wakati uliopita? (Ndiyo.) Hivyo uelewa wenu sasa basi ni wa kina zaidi? (Ndiyo.) Najua kwamba sasa watu wengi wananitarajia kusema ni nini hasa utakatifu wa Mungu, lakini Ninapozungumza kuhusu utakatifu wa Mungu Nitaongea kwanza kuhusu matendo ambayo Mungu anafanya. Nyinyi nyote mnapaswa kusikiza kwa makini, kisha nitawauliza utakatifu wa Mungu ni nini hasa. Sitawaeleza moja kwa moja, lakini badala yake nitawaacha mjaribu kuutambua, kuwapa nafasi ya kuutambua. Mnafikiri nini kuhusu mbinu hii? (Ni nzuri.) Kwa hivyo sikizeni kwa makini.

Wakati wowote Shetani anampotosha mwanadamu ama anashughulika na madhara yasiyodhibitiwa, Mungu hasimami bila kazi, wala haweke kando ama kupuuza wale ambao amechagua. Yote ambayo Shetani anafanya ni wazi kabisa na yanaeleweka na Mungu. Haijalishi anachofanya Shetani, haijalishi mwenendo anaosababisha kuibuka, Mungu anajua yote ambayo Shetani anajaribu kufanya, na Mungu hawawachi wale ambao amechagua. Badala yake, bila kuvuta macho hata kidogo, kwa siri, kwa ukimya, Mungu anafanya yote yanayohitajika. Mungu Anapoanza kufanya kazi kwa mtu, wakati amemchagua mtu, Haambii yeyote, wala Hamwambii Shetani, wala hata kufanya maonyesho makubwa. Anafanya tu kwa ukimya, kwa asili kile ambacho kinahitajika. Kwanza, Anakuchagulia familia; usuli ambao hiyo familia inao, wazazi wako ni nani, mababu zako ni nani—haya yote tayari yaliyamuliwa na Mungu. Kwa maneno mengine, haya hayakuwa uamuzi wa mvuto wa ghafla yaliyofanywa na Yeye, lakini badala yake hii ilikuwa kazi iliyoanza kitambo. Baada ya Mungu kukuchagulia familia, pia Anachagua tarehe ambayo utazaliwa. Kwa sasa, Mungu anaangalia unapozaliwa katika dunia hii ukilia, Anatazama kuzaliwa kwako, Anatazama unapotamka maneno yako ya kwanza, Anatazama unapoanguka na kutembea hatua zako za kwanza, ukijifunza kutembea. Kwanza unachukua hatua moja na kisha unachukua nyingine ... sasa unaweza kukimbia, sasa unaweza kuruka, sasa unaweza kuongea, sasa unaweza kuonyesha hisia zako. Mwanadamu anavyokuwa, macho ya Shetani yamewekwa

kwa kila mmoja wao, kama chui mkubwa mwenye milia anavyomwangalia nyara wake. Lakini kwa kufanya kazi Yake, Mungu hajawahi kuteseka mapungufu yoyote ya watu, matukio ama mambo, ya nafasi ama wakati; Anafanya kile anachopaswa kufanya na Anafanya kile Anacholazimika kufanya. Katika mchakato wa kukua, unaweza kukutana na mambo mengi ambayo hupendi, kukutana na magonjwa na kuvunjika moyo. Lakini unapotembea njia hii, maisha yako na bahati zako ziko chini ya ulinzi wa Mungu kabisa. Mungu anakupa hakikisho halisi litakalodumu maisha yako yote, kwani Yeye yuko kando yako, anakulinda na kukutunza. Bila kujua haya, unakua. Unaanza kukutana na mambo mapya na unaanza kujua dunia hii na wanadamu hawa. Kila kitu ni kipya kwako. Unapenda kufanya kile unachopenda. Unaishi katika ubinadamu wako mwenyewe, unaishi katika nafasi yako ya kuishi na huna hata kiasi kidogo cha mtazamo kuhusu kuwepo kwa Mungu. Lakini Mungu anakulinda katika kila hatua ya njia unapokua, na Anakutazama unapoweka kila hatua mbele. Hata unapojifunza maarifa, ama kusoma sayansi, Mungu hajawahi toka upande wako kwa hatua hata moja. Wewe ni sawa na watu wengine kwamba, katika harakati za kuja kujua na kukutana na dunia, umeanzisha mawazo yako mwenyewe, una mambo yako mwenyewe ya kupitisha muda, mambo unayopenda mwenyewe, na pia unayo matamano ya juu. Wakati mwingi unafikiria siku zako za baadaye, wakati mwingi ukichora muhtasari wa jinsi siku zako za baadaye zinapaswa kuwa. Lakini haijalishi kitakachofanyika njiani, Mungu anaona vyote na macho wazi. Labda wewe mwenyewe umesahau siku zako za nyuma, lakini kwa Mungu, hakuna anayeweza kukuelewa bora kuliko Yeye. Unaishi chini ya macho ya Mungu, unakua, unapevuka. Wakati huu, jukumu muhimu la Mungu ni kitu ambacho hakuna yeyote kamwe hufahamu, kitu ambacho hakuna yeyote anajua. Mungu hakika hakuambii kukihusu. Basi kitu hiki cha muhimu zaidi ni kipi? Inaweza kusemwa kwamba ni hakikisho kuwa Mungu atamwokoia mtu. Hii inamaanisha kwamba Mungu anataka kumwokoia mtu huyu, kwa hivyo lazima Afanye hivi, na kazi hii ni muhimu sana kwa mwanadamu na Mungu. Je, mnajua ni nini? Inaonekana kwamba hamna hisia yoyote kuhusu hili, ama dhana yoyote kuhusu hili, kwa hivyo nitawaambia. Kutoka ulipozaliwa hadi sasa, Mungu amefanya kazi nyingi sana kwako, lakini Hakupi maelezo moja baada ya nyingine ya kila kitu Amefanya. Mungu hakukuruhusu kujua, na Hakukwambia). Hata hivyo, kwa mwanadamu, kila kitu anachofanya Mungu ni muhimu. Kwa Mungu, ni kitu ambacho lazima Afanye. Katika moyo wake kuna kitu muhimu Anapaswa kufanya ambacho kinazidi yoyote ya mambo haya. Yaani, kutoka alipozaliwa mwanadamu hadi sasa, Mungu lazima ahakikishe usalama wao. Baada ya kusikia maneno haya, mnaweza kuhisi kana kwamba hamwelewi kikamilifu, kusema “usalama huu ni muhimu sana?” Kwa hivyo ni nini maana halisi ya “usalama”? Labda mnauelewa kumaanisha amani ama pengine mnauelewa kumaanisha kutopitia maafa ama msiba wowote, kuishi vyema, kuishi maisha ya kawaida. Lakini katika mioyo yenu lazima mjue kwamba si rahisi hivyo. Kwa hivyo ni nini hasa kitu hiki ambacho Nimekuwa nikizungumzia, ambacho

Mungu anapaswa kufanya? Usalama unamaanisha nini kwa Mungu? Kuna hakikisho lolote la usalama wenu? La. Kwa hivyo ni nini hiki ambacho Mungu anafanya? Usalama huu unamaanisha humezwi na Shetani. Je, jambo hili ni muhimu? Wewe humezwi na Shetani, kwa hivyo hili linahusisha usalama wako, au la? Hili linahusisha usalama wako binafsi, na hakuwezi kuwa na lolote muhimu zaidi. Baada ya wewe kumezwa na Shetani, nafsi yako wala mwili wako si vya Mungu tena. Mungu hatakuokoa tena. Mungu huacha nafsi kama hiyo na huacha watu kama hao. Kwa hivyo Nasema kitu muhimu sana ambacho Mungu anapaswa kufanya ni kuhakikishia usalama wako, kuhakikisha kwamba hutamezwa na Shetani. Hili ni muhimu kiasi, silo? Kwa hivyo mbona hamwezi kujibu? Inaonekana kwamba hamwezi kuhisi wema mkubwa wa Mungu!

Mungu anafanya mengi kando na kuhakikisha usalama wa watu, kuhakikisha kwamba hawatamezwa na Shetani; pia hufanya kazi nyingi sana kwa kutayarisha kumchagua mtu na kumwokoa. Kwanza, una tabia gani, utazaliwa kwa familia ya aina gani, wazazi wako ni nani, una kaka na dada wangapi, na hali, hadhi ya kiuchumi na tabia za familia ambayo unazaliwa ndani ni gani—haya yote yanapangiwa wewe kwa uangalifu na Mungu. Je, unajua ni familia ya aina gani watu waliochaguliwa na Mungu wanazaliwa ndani mara nyingi, kama inavyohusu watu wengi? Ni familia mashuhuri? Hatuwezi sema kwa uhakika hakuna yoyote. Kunaweza kuwa na nyingine, lakini kuna chache sana. Ni familia za utajiri wa kupindukia, kama yenye mabilioni ama yenye mamilioni nyingi? Mara nyingi huwa si aina hii ya familia. Kwa hivyo Mungu anapangia watu hawa familia za aina gani zaidi? (Familia za kawaida.) Kwa hivyo ni familia zipi ambazo zinaweza kufikiriwa za kawaida? Familia hizi ni pamoja na zile zinazofanya kazi—zinategemea mishahara yao kuishi na zinaweza kumudu mahitaji ya kimsingi na si wenye mali nyingi; pia ni pamoja na familia za ukulima. Wakulima hutegemea kupanda mazao kwa chakula chao, na wana nafaka za kula na nguo za kuvaa, hawataona njaa au kuhisi. Kisha kuna familia zingine zinazoendesha biashara ndogondogo, na zingine ambazo wazazi ni wenye akili, na hizi zinaweza kuhesabika kama familia za kawaida. Kuna baadhi ya wazazi ambao ni wafanyakazi wa ofisi ama maafisa wadogo wa serikali kwa kiwango zaidi, ambazo haziwezi kuhesabika kama familia mashuhuri pia. Watu wengi zaidi wanazaliwa katika familia za kawaida, na haya yote yanapangiliwa na Mungu. Kusema kwamba, kwanza kabisa mazingira haya unayoishi si familia ya uwezo mkubwa ambayo unaweza kufikiria, lakini badala yake ni familia uliyoamuliwa na Mungu, na watu wengi wataishi katika mipaka ya aina hii ya familia. Kwa hivyo je, hadhi ya kijamii? Hali ya uchumi ya wengi wa wazazi ni wastani na hawana hadhi ya juu ya kijamii—kwao ni vizuri tu kuwa na kazi. Kuna wowote walio magavana? Kuna wowote walio maraisi? (La.) Kwa zaidi ni watu kama mameneja wa biashara ndogo ama wakubwa wa muda mfupi. Hadhi zao za kijamii ni kuwa katikati, na hali zao za uchumi ni wastani. Sababu nyingine ni

mazingira ya kuishi ya familia. Kwanza kabisa, hakuna wazazi ambao wanaweza kushawishi kwa wazi watoto wao kutembea njia ya uaguzi na kupiga ramli; hawa pia ni wachache. Wazazi wengi ni wa kawaida kiasi. Mungu anaweka mazingira ya aina hii kwa ajili ya watu wakati sawa na kuwachagua, na ni kwa manufaa sana ya kazi Yake ya kuokoa watu. Kwa nje, inaonekana kwamba Mungu hajafanya chochote kikuu kwa mwanadamu; Anafanya kila kitu kwa siri tu, kwa unyenyekevu na kwa kimya. Lakini kwa hakika, vyote ambavyo Mungu anafanya vinafanywa kuweka msingi wa wokovu wako, kuandaa njia mbeleni na kuandaa hali zote muhimu za wokovu wako. Halafu, Mungu anawarudisha mbele Yake, kila mtu kwa wakati wake: Ni wakati huo ndipo unaposikia sauti ya Mungu; ni wakati huo ndipo unapokuja mbele Yake. Kufikia wakati hilo linafanyika, watu wengine wamekuwa wazazi tayari wenyewe, ilhali wengine bado ni watoto wa mtu tu. Kwa maneno mengine, watu wengine wameoa na kupata watoto ilhali wengine bado hawajaoa, na hawajaanza bado familia zao. Lakini licha ya hali za watu, Mungu tayari ameweka nyakati utakapochaguliwa na injili na maneno Yake yatakapokufikia. Mungu ameweka hali, ameamulia mtu fulani ama muktadha fulani ambamo injili itapitishwa kwako, ili uweze kusikia maneno ya Mungu. Mungu tayari amekuandalia hali zote muhimu ili, bila kujua, unakuja mbele Yake na unarudishwa kwa familia ya Mungu. Pia, bila kujua, unafuata Mungu na kuingia katika kazi Yake ya hatua kwa hatua, kuingia katika kila hatua ya njia ya Mungu ya kazi ambayo ameandalia mwanadamu. Ni njia za aina gani ambazo Mungu hutumia wakati Anapofanya mambo kwa ajili ya mwanadamu wakati huu? Kwanza, angalau kabisa ni utunzaji na ulinzi ambao mwanadamu hufurahia. Kando na hayo, Mungu huweka watu, matukio, na vitu mbalimbali ili mwanadamu aweze kuona kuwepo Kwake na matendo Yake miongoni mwao. Kwa mfano, kuna watu wengine wanaomwamini Mungu kwa sababu mtu katika familia yao ni mgonjwa. Wakati wengine wanawahubiria injili, wanaanza kumwamini Mungu, na imani hii kwa Mungu imekuja kwa sababu ya hali hii. Kwa hivyo ni nani aliyepangilia hali hii? (Mungu.) Kwa njia ya maradhi haya, kuna familia zingine ambamo wote ni waumini, vijana na wazee, ilhali kuna familia zingine ambamo imani ni ya kibinafsi. Inavyoonekana, mtu katika familia yako ana maradhi, lakini kwa hakika ni hali uliyopewa ili uje mbele ya Mungu—huu ni wema wa Mungu. Kwa sababu maisha ya familia ya watu wengine ni magumu na hawawezi kupata amani yoyote, fursa ya bahati inakuja ambapo mtu anapitisha injili na kusema, “Mwamini Bwana Yesu na utakuwa na amani.” Bila fahamu, basi anakuja kumwamini Mungu katika hali asili, kwa hivyo hii si aina ya hali? Na je, familia yake kuwa na amani si neema aliyopewa na Mungu? Kisha kuna wengine wanaokuja kumwamini Mungu kwa sababu zingine. Kuna sababu tofauti na njia tofauti za imani, lakini licha ya sababu inakuleta kumwamini Yeye, yote hakika yamepangwa na kuongozwa na Mungu. Kwanza, Mungu hutumia njia kadhaa ili kukuchagua na kukuleta katika familia Yake. Hii ndiyo neema Mungu anayompa kila mwanadamu.

Sasa na kazi ya Mungu katika siku za mwisho, Hampi tena mwanadamu neema na baraka tu kama Alivyofanya awali, wala halazimishi watu kwenda mbele. Wakati wa hatua hii ya kazi, ni nini mwanadamu ameona kutoka kwa vipengele hivi vyote vya kazi ya Mungu ambavyo wamepitia? Wameona upendo wa Mungu, na hukumu na kuadibu kwa Mungu. Kwa wakati huu, Mungu zaidi ya hayo, anamtegemeza, tia nuru, na kumwongoza mwanadamu, ili aje kujua nia Zake polepole, kujua maneno Anayozungumza na ukweli Anaompa mwanadamu. Wakati mwanadamu ni mnyonge, wakati amevunjika roho, wakati hana popote pa kugeukia, Mungu atatumia maneno Yake kufariji, kushauri na kuwatia moyo, ili mwanadamu wa kimo kidogo aweze kupata nguvu polepole, kuinuka kwa wema na kuwa radhi kushirikiana na Mungu. Lakini wakati wanadamu hawamtii Mungu ama wanampinga Yeye, ama wanapofichua upotovu wao, Mungu hataonyesha huruma kuwarudi na kuwafundisha nidhamu. Kwa ujinga, kutojua, unyonge, na uchanga wa mwanadamu, hata hivyo, Mungu ataonyesha uvumilivu na ustahimilivu. Kwa njia hii, kupitia kazi yote Mungu anamfanyia mwanadamu, mwanadamu anapevuka, anakua na anakuja kujua nia za Mungu polepole, kujua baadhi ya ukweli, kujua ni nini mambo mema na ni nini mambo hasi, kujua uovu ni nini na kujua giza ni nini. Mungu hamrudi na kumfundisha nidhamu mwanadamu siku zote wala Haonyeshi uvumilivu na ustahimilivu siku zote. Badala yake anampa kila mtu kwa njia tofauti, katika hatua zao tofauti na kulingana na kimo na ubora wa tabia yao tofauti. Anamfanyia mwanadamu mambo mengi na kwa gharama kubwa; mwanadamu hafahamu lolote la gharama hii ama mambo haya Mungu anafanya, ilhali yote ambayo anafanya kwa kweli inafanywa kwa kila mtu. Upendo wa Mungu ni wa kweli: Kupitia neema ya Mungu mwanadamu anaepuka janga moja baada ya jingine, ilhali kwa unyonge wa mwanadamu, Mungu anaonyesha ustahimili wake muda baada ya muda. Hukumu na kuadibu kwa Mungu yanaruhusu watu kuja kujua polepole upotovu wa wanadamu na kiini chao cha kishetani. Kile ambacho Mungu anapeana, kutia nuru Kwake kwa mwanadamu na uongozi Wake yote yanawaruhusu wanadamu kujua zaidi na zaidi kiini cha ukweli, na kujua zaidi kile ambacho watu wanahitaji, njia wanayopaswa kuchukua, kile wanachoishia, thamani na maana ya maisha yao, na jinsi ya kutembea njia iliyo mbele. Haya mambo yote ambayo Mungu anafanya hayatengwi na lengo Lake la awali. Ni nini, basi lengo hili? Mbona Mungu anatumia njia hizi kufanya kazi Yake kwa mwanadamu? Anataka kutimiza matokeo gani? Kwa maneno mengine, ni nini ambacho anataka kuona kwa mwanadamu na kupata kutoka kwake? Kile ambacho Mungu anataka kuona ni kwamba moyo wa mwanadamu unaweza kufufuliwa. Njia hizi ambazo anatumia kufanya kazi kwa mwanadamu ni za kuamsha bila kikomo moyo wa mwanadamu, kuamsha roho ya mwanadamu, kumwacha mtu kujua alipotoka, ni nani anayemwongoza, kumsaidia, kumkimu, na ni nani ambaye amemruhusu mwanadamu kuishi hadi sasa; ni ya kuwacha mwanadamu kujua ni nani Muumbaji, ni nani wanapaswa kuabudu, ni njia gani wanapaswa kutembelea, na mwanadamu anapaswa kuja mbele ya Mungu kwa njia gani;

yanatumika kufufua moyo wa mwanadamu polepole, ili mwanadamu ajue moyo wa Mungu, aelewe moyo wa Mungu, na aelewe utunzaji mkuu na wazo nyuma ya kazi Yake kumwoko mwanadamu. Wakati moyo wa mwanadamu umefufuliwa, hataki tena kuishi maisha ya uasherati, tabia potovu, lakini badala yake kutaka kufuatilia ukweli kwa kuridhishwa kwa Mungu. Wakati moyo wa mwanadamu umeamshwa, anaweza basi kujinusuru kutoka kwa Shetani, kutoathiriwa tena na Shetani, kutodhibitiwa na kudanganywa na yeye. Badala yake, mwanadamu anaweza kushiriki kwa makini katika kazi ya Mungu na maneno Yake ili kuridhisha moyo wa Mungu, na hivyo kupata uchaji wa Mungu na kuepuka uovu. Hili ndilo lengo la awali la kazi ya Mungu.

Kuzungumza kuhusu uovu wa Shetani hivi sasa kulimfanya kila mtu kuhisi kana kwamba watu huishi kwa huzuni sana na kwamba maisha ya mwanadamu yamejaa bahati mbaya. Lakini mnahisi vipi sasa kwani Nimezungumza kuhusu utakatifu wa Mungu na kazi ambayo anafanya kwa mwanadamu? (Furaha sana.) Tunaweza kuona sasa kwamba kila kitu Mungu anafanya, kila kitu ambacho anapanga kwa uangalifu kwa mwanadamu ni safi kabisa. Kila kitu anachofanya Mungu ni bila kasoro, kumaanisha ni bila dosari, hakihitaji yeyote kukosoa, kutoa mawaidha ama kufanya mabadiliko yoyote. Kila kitu ambacho Mungu anafanya kwa kila mtu hakina shaka; Anaongoza kila mtu kwa mkono, Anakuchunga kwa kila muda na Hajawahi kuondoka upande wako. Watu wanapokua katika mazingira haya na kukua na usuli wa aina hii, tunaweza kusema kwamba watu kwa kweli wanakua katika kiganja cha mkono wa Mungu? (Ndiyo.) Kwa hivyo sasa bado mnahisi hisia za hasara? Je, kuna yeyote anayehisi kuvunjika moyo bado? Kuna yeyote anayehisi kwamba Mungu amewaacha wanadamu? (La.) Kwa hivyo ni nini hasa Mungu amefanya? (Anawahifadhi wanadamu.) Wazo na utunzaji mkuu nyuma ya kila anachofanya Mungu hayapingwi. Hata zaidi, wakati Mungu anapofanya kazi Yake, hajawahi kuweka sharti ama mahitaji yoyote kwa yeyote kati yenu kujua gharama anayokulipia, kwa hivyo uishi shukrani kwake kwa kina. Je, Mungu amewahi kufanya chochote kama hiki kabla? (La.) Katika miaka yenu mirefu yote, kimsingi kila mtu amekutana na hali nyingi hatari na kupitia majaribu mengi. Hii ni kwa sababu Shetani yupo kando yako, macho yake yakikutazama kila wakati. Anapenda janga linapokupata, wakati maafa yanakupata, wakati hakuna chochote kinaenda sawa kwako, na anapendelea unaponaswa na wavu wa Shetani. Kuhusu Mungu, anakulinda kila wakati, kukuweka mbali na bahati moja mbaya baada ya nyingine na kutokana na janga moja baada ya jingine. Hii ndiyo maana Nasema kwamba kila kitu ambacho mwanadamu anacho—amani na furaha, baraka na usalama wa kibinafsi—yote hakika yanadhibitiwa na Mungu, na Anaongoza na kuamua hatima ya kila mtu. Lakini, je, Mungu ana dhana iliyovimbishwa ya cheo chake, kama wanavyosema watu wengine? Kukuambia “Mimi ni mkuu kabisa wa wote, ni Mimi ninayechukua watamu wenu, lazima nyote mniombe huruma na kutotii kutaadhibiwa na kifo.”

Je, Mungu amewahi kutishia wanadamu kwa njia hii? (La.) Ashawahi kusema “Wanadamu ni wapotovu kwa hivyo haijalishi Ninavyowashughulikia, utendeaji wowote holela utatosha; Silitaji kupanga mambo vizuri sana kwa sababu yao.” Je, Mungu anafikiria kwa njia hii? Mungu ametenda kwa njia hii? (La.) Kinyume na haya, utendeaji wa Mungu wa kila mtu ni wenye ari na ambao umewajibika, umewajibika zaidi hata kuliko vile ulivyo kwa wewe mwenyewe. Sivyo hivi? Mungu haongei bure, wala hasimami juu akijifanya kuwa muhimu wala hadanganyi watu. Badala yake, Anafanya vitu ambavyo Yeye Mwenyewe anapaswa kufanya kwa uaminifu na kwa ukimya. Mambo haya yanaleta baraka, amani na furaha kwa mwanadamu. Yanamleta mwanadamu kwa amani na kwa furaha katika macho ya Mungu na ndani ya familia Yake; kisha wanaishi mbele ya Mungu na kukubali wokovu wa Mungu na fikira na mawazo ya kawaida. Kwa hivyo Mungu amewahi kuwa mdanganyifu kwa mwanadamu katika kazi Yake? Ashawahi kuonyesha maonyesho ya uongo ya ukarimu, Akimpumbaza mwanadamu na mazungumzo ya kufurahisha, kisha kumpuuza mwanadamu? (La.) Je, Mungu ashawahi kupeana ahadi tupu na kujigamba, Akikuambia kwamba Anaweza kukufanyia hili ama kukusaidia kufanya lile, na kisha kutoweka? (La.) Hakuna udanganyifu ndani ya Mungu, hakuna uongo. Mungu ni mwaminifu na kila kitu Anachofanya ni halisi. Ni Yeye pekee ambaye watu wanaweza kutegemea na Mungu ambaye watu wanaweza kuaminia maisha yao na yote wanayo Kwake. Kwa vile hakuna udanganyifu ndani ya Mungu, tunaweza kusema kwamba Mungu ndiye wa kweli zaidi? (Ndiyo.) Bila shaka tunaweza, siyo? Ingawa, kuzungumza kuhusu maneno haya sasa, likitumika kwa Mungu ni dhaifu sana, cha ubinadamu sana, hakuna lolote tunaloweza kufanya kulihusu kwa vile hii ni mipaka ya lugha ya binadamu. Si sahihi sana hapa kumwita Mungu wa kweli, lakini tutatumia neno hili kwa sasa. Mungu ni mwaminifu. Kwa hivyo tunamaanisha nini kwa kuongea kuhusu vipengele hivi? Je, tunamaanisha tofauti kati ya Mungu na mwanadamu na tofauti kati ya Mungu na Shetani? Tunaweza kusema hivi. Hii ni kwa sababu mwanadamu hawezi kuona chembe cha tabia potovu ya Shetani kwa Mungu. Je, Niko sahihi kusema hivi? Ninaweza kupata Amina kwa sababu ya hili? (Amina!) Hatuoni uovu wowote wa Shetani ukifichuliwa kwa Mungu. Yote ambayo Mungu hufanya na kufichua ni muhimu sana na ya msaada sana kwa mwanadamu, yanafanywa kumkimu mwanadamu kabisa, yamejaa uhai na yanampa mwanadamu njia ya kufuata na mwelekeo wa kuchukua. Mungu hajapotoka, na zaidi ya hayo, kuangalia sasa kila kitu Mungu hufanya, tunaweza kusema kwamba Mungu ni mtakatifu? (Ndiyo.) Kwa sababu Mungu hana upotovu wowote wa mwanadamu na hana chochote sawa na, au kinachofanana na tabia potovu ya mwanadamu ama kiini cha Shetani, kutoka mtazamo huu tunaweza kusema kwamba Mungu ni mtakatifu. Mungu hafichui upotovu wowote, na ufunuo wa kiini Chake katika kazi Yake yote ni thibitisho tunalohitaji kwamba Mungu Mwenyewe ni mtakatifu. Je, mnaona hili? Sasa, kujua asili takatifu ya Mungu, kwa sasa wacha tuangalie hivi vipengele

viwili: 1) Hakuna tabia potovu ndani ya Mungu; 2) kiini cha kazi ya Mungu kwa mwanadamu kinamruhusu mwanadamu kuona kiini cha Mungu mwenyewe na kiini hiki ni kizuri kabisa. Kwa kuwa vitu ambavyo kila namna ya kazi ya Mungu inamletea mwanadamu ni vitu vizuri. Kwanza, Mungu anamhitaji mwanadamu kuwa mwaminifu—hili si zuri? Mungu anampa mwanadamu maarifa—hili si zuri? Mungu anamfanya mwanadamu aweze kutambua kati ya mema na maovu—hili si zuri? Anamruhusu mwanadamu kuelewa maana na thamani ya maisha ya binadamu—hili si zuri? Anamruhusu mwanadamu kuona ndani ya kiini cha watu, matukio na mambo kulingana na ukweli—hili si zuri? (Ndiyo ni zuri.) Na matokeo ya haya yote ni kwamba mwanadamu hadanganywi tena na Shetani, haendelei kudhuriwa na Shetani ama kudhibitiwa na yeye. Kwa maneno mengine, yanawaruhusu watu kujinusurisha kabisa kutoka upotovu wa Shetani, na hivyo kutembea polepole njia ya kumcha Mungu na kuepuka maovu. Mmetembea umbali gani katika njia hii sasa? Ni vigumu kusema, sivyo? Lakini angalau sasa mna uelewa wa mwanzo wa jinsi Shetani anampotosha mwanadamu, vitu vipi ni ovu na vitu vipi ni hasi? Nyinyi angalau mnatembea sasa njia sahihi. Je, tunaweza kusema hivyo? (Ndiyo.)

Tutamaliza sasa kuzungumzia kuhusu utakatifu wa Mungu, kwa hivyo nani miongoni mwenu, kutoka yote ambayo mmesikia na kupokea, anaweza kusema utakatifu wa Mungu ni nini? Utakatifu wa Mungu ninaozungumzia unarejelea nini? Lifikirie kidogo. Je, ukweli wa Mungu ni utakatifu Wake? Je, uaminifu wa Mungu ni utakatifu Wake? Je, kutokuwa na ubinafsi kwa Mungu ni utakatifu Wake? Je, unyenyekevu wa Mungu ni utakatifu Wake? Je, upendo wa Mungu kwa mwanadamu ni utakatifu Wake? Mungu humpa mwanadamu ukweli na uhai bure—huu ni utakatifu Wake? (Ndiyo.) Yote haya ambayo Mungu anafichua ni wa kipekee; hayapo katika binadamu potovu, wala hayawezi kuonekana hapo. Hakuna hata chembe ya hayo yanaweza kuonekana katika mchakato wa upotovu wa Shetani wa mwanadamu, wala katika tabia potovu ya Shetani wala katika kiini ama asili ya Shetani. Chote ambacho Mungu Anacho na Alichu ni ya kipekee na Mungu tu Mwenyewe anacho kiini cha aina hii, ni Mungu Mwenyewe tu anamiliki kiini cha aina hii. Baada ya kuzungumza hili hadi sasa, kuna yeyote kati yenu ambaye ameona yeyote mtakatifu hivi miongoni mwa wanadamu? (La.) Kwa hivyo, kuna yeyote mtakatifu hivi miongoni mwa watu maarufu, watu wakuu na mashuhuri mnaoabudu katika ubinadamu? (La.) Kwa hivyo sasa tunasema kwamba utakatifu wa Mungu ni wa kipekee, je anadhihirisha hili katika jina na vile vile katika ukweli? (Ndiyo.) Anadhihirisha. Zaidi ya hayo, kuna pia sehemu yake ya utendaji. Je, kuna tofauti zozote kati ya utakatifu ninaozungumzia sasa na utakatifu ambao mlifikiria na kudhania awali? (Ndiyo.) Kwa hivyo tofauti hii ni kubwa kiasi gani? (Kubwa sana!) Watu humaanisha nini sanasana wanapoongea kuhusu utakatifu huu? (Baadhi ya tabia ya nje.) Tabia, ama kama njia ya kuelezea kitu, wanasema kwamba ni takatifu. Ni kitu tu kinachoonekana kuwa safi na kizuri, kitu

kinachoonekana ama kusikika kuwa kizuri kwa watu, si chochote cha asili yoyote halisi ya utakatifu. Hii ni dhahania. Kando ya hili, kipengele cha utendaji cha “utakatifu” ambacho watu wanafikiria kinarejelea nini hasa? Je hasa ni kile wanachokifikiria ama kudhania kuwa? Kwa mfano, Wanabudhaa wengine hufariki wakati wanatia vitendoni, wanaaga wakiwa wamekaa pale wakilala. Watu wengine husema kwamba wamekuwa watakatifu na kuruka mbinguni. Hii pia ni aina ya ubunifu. Pia kuna wengine ambao wanafikiria kwamba kichimbakazi anayeelea chini kutoka mbinguni ni mtakatifu. Kwa kweli, wazo la watu la neno “takatifu” limekuwa tu kama fikira tupu na dhahania ambayo kimsingi haina kiini, na zaidi ya hayo haina chochote kuhusu kiini cha utakatifu. Kiini cha utakatifu ni upendo wa kweli, lakini hata zaidi ya hili ni kiini cha ukweli, cha haki na mwanga. Neno “takatifu” linafaa tu linapotumika kwa Mungu; hakuna chochote katika uumbaji kinachostahiki kuitwa takatifu. Mwanadamu lazima aelewe hilo. Kuanzia sasa kuendelea, tunatumia neno “takatifu” kwa Mungu pekee. Hii ni ya kufaa? (Ndiyo, inafaa.)

Hebu turudi kuzungumza kuhusu mbinu ambazo Shetani hutumia kumpotosha mwanadamu. Tumeongea karibuni kuhusu mbinu mbalimbali ambazo Mungu anafanya kazi kwa mwanadamu na ambazo kila mmoja wenu anaweza kupitia mwenyewe, kwa hivyo sitatoa maelezo zaidi. Lakini katika mioyo yenu pengine mmechanganyikiwa kuhusu mbinu ambazo Shetani hutumia kumpotosha mwanadamu, ama kwa kiwango cha chini zaidi ana upungufu wa maelezo. Ni ya manufaa kwenu kwa Mimi kuzungumzia hili tena? (Ndiyo.) Je, mnataka kumwelewa? Pengine wengine wenu watauliza: “Mbona tuzungumze kuhusu Shetani tena? Punde tunapoongea kuhusu Shetani, tunakuwa na hasira, na tunaposikia jina lake tunahisi kutotulia kila mahali.” Bila kujali jinsi anavyokufanya kutotulia, lazima ukubali ukweli, na mambo haya yanapaswa kuzungumziwa kwa uwazi na kufanywa dhahiri kwa manufaa ya ufahamu wenu: kama sivyo hamwezi kweli kuepukana na ushawishi wa Shetani.

Tumezungumza hapo awali njia tano ambazo Shetani anatumia kumpotosha mwanadamu. Ndani ya hizi njia tano kuna mbinu anazotumia. Njia ambazo Shetani anampotosha mwanadamu ni aina ya kifuniko tu; ya kudhuru kwa siri zaidi ni mbinu zinazojificha nyuma ya sura hii ya kinafiki na anataka kutumia mbinu hizi kufikia malengo yake. Mbinu hizi ni zipi? Nipeni muhtasari. (Anadanganya, anashawishi na anatishia.) Kadri mnavyoendelea kutaja ndivyo mnavyokaribia. Inaonekana kana kwamba mmedhuriwa kwa kina na yeye na mna hisia kali kuhusu mada hii. (Anatumia pia maneno matamu, anashawishi, na anamiliki kwa nguvu.) Anamiliki kwa nguvu—hii inatoa fikra ya kina. Watu wanaogopa umiliki wa nguvu wa Shetani, siyo? Kuna mengine? (Huwadhuru watu kikatili, hutumia vitisho na vivutio, na hudanganya.) Uongo ni kiini cha matendo yake na hudanganya ili kukulaghai. Ni nini asili ya kudanganya? Je, kudanganya si sawa na kulaghai? Lengo la kusema uongo kwa kweli ni kukudanganya wewe. Je,

kuna ujanja mwingine? Niambieni njia zote ujanja wa Shetani mnazojua. (Yeye hushawishi, hudhuru, hupofusha na hudanganya.) Wengi wenu mnahisi sawa kuhusu uongo huu, sivyo? (Yeye humdhibiti mwanadamu, humkamata mwanadamu, humtishia sana mwanadamu na humzuia mwanadamu kumwamini Mungu.) Ninajua vizuri kiasi mnachomaanisha na yote ni mazuri. Nyote mnajua kitu kuhusu hili, kwa hivyo wacha sasa tufanye muhtasari.

Kuna njia sita za msingi ambazo Shetani hutumia kumpotosha mwanadamu.

Ya kwanza ni kudhibiti na kulazimisha. Yaani, Shetani atafanya vyovyote vile kudhibiti moyo wako. “Kulazimisha” kunamaanisha nini? Kunamaanisha kutumia mbinu za kutishia na kulazimisha kukufanya umtii, kukufanya kufikiria matokeo usipomtii. Unaogopa na huthubutu kumpinga, kwa hivyo basi unamtii.

Ya pili ni kudanganya na kulaghai. “Kudanganya na kulaghai” yanahusisha nini? Shetani hutunga baadhi ya hadithi na uongo, kukulaghai wewe kuziamini. Hakwambii kamwe kwamba mwanadamu aliumbwa na Mungu, wala hasemi pia moja kwa moja kwamba hukuumbwa na Mungu. Hatumii jina “Mungu” kabisa, lakini badala yake hutumia kitu kingine mbadala, akitumia kitu hiki kukudanganya ili kimsingi usiwe na wazo la kuwepo kwa Mungu. Huu ulaghai bila shaka unahusisha vipengele vingi, sio tu hiki kimoja.

Ya tatu ni kufunza kwa nguvu. Kufunza nini kwa nguvu? Je, kufunzwa kwa nguvu kunafanywa kwa hiari ya mwanadamu mwenyewe? Je, kunafanywa na idhini ya mwanadamu? (La.) Haijalishi kama hukuidhinisha. Katika kutojua kwako, humwaga ndani yako, kuweka ndani yako kufikiria kwa Shetani, kanuni zake za maisha na kiini chake.

Ya nne ni vitisho na vivutio. Yaani, Shetani hutumia mbinu mbalimbali ili umkubali, umfuata, ufanye kazi katika Huduma yake; hujaribu kufikia malengo yake kwa vyovyote vile. Saa zingine hukupa fadhili ndogo lakini bado hukushawishi kufanya dhambi. Usipomfuata, atakufanya uteseke na kukuadhibu na atatumia njia mbalimbali kukushambulia na kukutega.

Ya tano ni uongo na kiharusi. “Uongo na kiharusi” ni kwamba Shetani hutunga kauli na mawazo yanayosikika kuwa matamu ambayo yako pamoja na dhana za watu kufanya ionekane kwamba anatilia maanani miili ya watu ama anafikiria kuhusu maisha yao na siku zao za baadaye, wakati hakika anakudanganya tu. Kisha anakupooza ili usijue kile kilicho sahihi na kile kilicho makosa, ili udanganywe bila kujua na hivyo kuja chini ya udhibiti wake.

Ya sita ni maangamizi ya mwili na akili. Shetani huharibu kipi cha mwanadamu? (Akili yao, nafsi yao yote.) Shetani huharibu akili yako, kukufanya kutokuwa na nguvu za kupinga, kumaanisha kuwa polepole sana moyo wako unageuka kwa Shetani licha ya wewe mwenyewe.

Huingiza mambo haya ndani yako kila siku, kila siku akitumia mawazo na utamaduni huu kukushawishi na kukuelimisha, polepole akiharibu utashi wako, kukufanya kutotaka kuwa mtu mzuri tena, kukufanya kutotaka tena kuvumilia katika kutetea kile unachoita cha haki. Bila kujua, huna tena utashi wa kuogelea kinyume na mkondo dhidi ya bamvua, lakini badala yake kububujika chini pamoja nayo. “Maangamizi” yanamaanisha kwamba Shetani hutesa watu sana hadi wanakuwa vivuli vya wao wenyewe, sio wanadamu tena. Hapa ndipo Shetani huwapiga, kuwashika na kuwameza.

Kila ya hizi njia zote Shetani hutumia kumpotosha mwanadamu inaweza kumfanya mwanadamu kutokuwa na nguvu ya kupinga; yoyote inaweza kuwa ya kufisha kwa watu. Kwa maneno mengine, chochote anachofanya Shetani na njia yoyote anayotumia inaweza kukufanya kupotoka, inaweza kukuleta chini ya udhibiti wa Shetani na inaweza kukuzamisha katika bwawa la uovu. Hizi ndizo njia Shetani hutumia kumpotosha mwanadamu.

Tunaweza kusema Shetani ni mwovu, lakini ili kuthibitisha hili ni lazima bado tuangalie matokeo ya upotovu wa Shetani wa mwanadamu ni yapi na ni tabia gani na viini vipi anamletea mwanadamu. Nyote mnajua kitu kuyahusu, kwa hivyo ongeeni. Matokeo ya upotoshaji wa Shetani kwa watu ni yapi? Wao hufichua tabia gani potovu? (Kiburi na majivuno, ubinafsi na kustahili dharau, uovu na udanganyifu, kudhuru kwa siri na kijicho, na utovu wa ubinadamu.) Kwa ujumla, tunaweza kusema hazina ubinadamu, siyo? Wacha kaka na dada wengine wazungumze. (Punde mwanadamu anapopotoshwa na Shetani, wakati mwingi hasa huwa mwenye kiburi na wa kujidai, wa kujigamba na mwenye majivuno, mwenye tamaa na mwenye ubinafsi. Haya ndiyo mazito sana.) (Baada ya mwanadamu kupotoshwa na Shetani, anafanya chochote ili kupata mali na utajiri. Kisha wanakua wakatili kwa Mungu, wanampinga Mungu, hawamtii Mungu, na anapoteza dhamiri yake na akili ambayo mwanadamu anapaswa kumiliki.) Yale ambayo mmesema yote kimsingi ni sawa na ijapokuwa na tofauti kidogo tu; wengine wenu mmeongeza maelezo madogo kiasi. Kwa muhtasari, mambo yanayojitokeza kuhusu binadamu wapotovu ni kiburi, udanganyifu, kuwa mwenye kijicho na ubinafsi. Hata hivyo, nyote mmepuuza kitu sawa. Watu hawana dhamiri, wamepoteza akili zao na hawana ubinadamu—lakini kitu kingine muhimu zaidi ambacho hamjataja, ambacho ni “usaliti”. Matokeo ya mwisho ya tabia hizi ambazo zipo kwa mwanadamu yeyote baada ya kupotoshwa na Shetani ni kusaliti kwao Mungu. Licha ya kile Mungu anamwambia mwanadamu ama licha ya kazi anayomfanyia, hatilii maanani kile ambacho anajua kuwa ukweli, yaani, hamtambui Mungu tena na anamsaliti: Haya ndiyo matokeo ya upotovu wa Shetani wa mwanadamu. Ni sawa kwa tabia zote potovu za mwanadamu. Miongoni mwa njia ambazo Shetani hutumia kumpotosha mwanadamu—maarifa ambayo mwanadamu hujifunza, sayansi anayojua, ushirikina, utamaduni wa jadi, na mitindo ya kijamii anayoelewa—kuna yoyote ambayo mwanadamu anaweza kutumia kusema kile kilicho

haki na kile kisicho haki? Kuna chochote kinachoweza kumsaidia mwanadamu kujua kilicho takatifu na kilicho ovu? Kuna viwango vyovyote? (La.) Hakuna viwango na hakuna msingi ambao unaweza kumsaidia mwanadamu. Hata kama watu wanajua neno “takatifu,” hakuna yeyote anayejua kweli kile kilicho takatifu. Kwa hivyo mambo haya ambayo Shetani anamletea mwanadamu yanaweza kumruhusu kujua ukweli? Je, yanaweza kumruhusu mwanadamu kuishi na ubinadamu unaoongezeka? Je, yanaweza kumruhusu mwanadamu kuishi maisha ambamo anaweza zaidi na zaidi kumwabudu Mungu? (La.) Ni dhahiri kwamba hayawezi kumruhusu mwanadamu kumwabudu Mungu, au kuelewa ukweli, wala hayawezi kumruhusu mwanadamu kujua utakatifu na uovu ni nini. Kinyume chake, mwanadamu anakuwa zaidi na zaidi mwenye uasherati, mbali na mbali zaidi na Mungu. Hii ndiyo sababu ya mbona tunasema Shetani ni mwovu. Baada ya kuchangua asili ovu nyingi za Shetani, je, mmeona Shetani kuwa na dalili yoyote ya utakatifu katika sifa zake ama katika uelewa wenu wa kiini chake? (La.) Hiyo ni ya hakika. Kwa hivyo mmeona kiini chochote cha Shetani ambacho kinashiriki usawa wowote na Mungu? (La.) Je, kuna maonyesho ya Shetani ambayo yanashiriki usawa na Mungu? (La.) Kwa hivyo sasa Nataka kuwauliza, kwa kutumia maneno yenu, utakatifu wa Mungu ni nini hasa? Kwanza kabisa, utakatifu wa Mungu unasemwa kwa uhusiano na nini? Je, unasemwa kwa uhusiano na kiini cha Mungu? Ama unasemwa kwa uhusiano na vipengele fulani vya tabia Yake? (Inasemwa kwa uhusiano na kiini cha Mungu.) Lazima tupate kidato wazi katika mada yetu tunayopenda. Inasemwa kwa uhusiano wa kiini cha Mungu. Kwanza kabisa, tumetumia uovu wa Shetani kama foili^[a] ya kiini cha Mungu, kwa hivyo umeona kiini chochote cha Shetani katika Mungu? (La, hatujaona). (Mungu si fidhuli, si mchoyo na hasaliti, na kutokana na kipengele hiki kiini kitakatifu cha Mungu kinaonekana kufumbuliwa. Kunacho kingine cha kuongeza? (Mungu hana dalili za tabia potovu ya Shetani. Chochote Shetani anacho ni hasi kabisa, wakati kile ambacho Mungu anacho ni kizuri. Tunaweza kuona kwamba Mungu amekuwa upande wetu daima, Akitulinda na kutuhifadhi kutoka wakati tulipokuwa wachanga, katika maisha yetu yote hadi sasa, na hasa wakati ambapo tumechanganyikiwa na kupotea njia. Hamna udanganyifu ndani ya Mungu, hamna kusema uongo. Yeye hunena kwa udhahiri na uwazi, na hii pia ni asili ya kweli ya Mungu.) Vizuri sana! (Hatuwezi kuona tabia yoyote potovu ya Shetani kwa Mungu, hamna udanganyifu, hamna kujisifu, hamna ahadi tupu na hamna udanganyifu. Ni Mungu pekee ambaye mwanadamu anaweza kuamini na Mungu ni mwaminifu na mkweli. Kutoka kwa kazi ya Mungu, tunaweza kuona Mungu akiwaambia watu wawe waaminifu, wawe na hekima, wawe na uwezo wa kung’amua kati ya mema na mabaya na kuwa na utambuzi wa watu, matukio, na mambo mbalimbali. Kwa haya tunaweza kuona utakatifu wa Mungu.) Je, mmemaliza? Je, mmeridhika na mliyoyasema? Ni kiasi gani cha uelewa cha Mungu kweli upo mioyoni mwenu? Na mnaelewa kiasi kipi utakatifu wa Mungu? Najua kwamba kila mmoja kati yenu katika moyo wake ana baadhi ya kiwango cha ufahamu wa utambuzi, kwa

sababu kila mtu anaweza kuhisi kazi ya Mungu kwao na, katika viwango tofauti, wao hupata vitu vingi kutoka kwa Mungu; wao hupata neema na baraka, wao hutwa nuru na kuangaziwa, na wao hupokea hukumu na kuadibu kwa Mungu ili kwamba mwanadamu aweze kuwa na uelewa rahisi wa kiini cha Mungu.

Ingawa utakatifu wa Mungu tunaoadili leo unaweza kuonekana geni kwa watu wengi, bila kujali jinsi unaweza kuonekana tumeanza mada hii, na mtakuwa na ufahamu zaidi mnapotembea katika njia yenu kwenda mbele. Itawalazimu kuja kuhisi na kuelewa kutoka kwa uzoefu wenu wenyewe kwa utaratibu. Sasa uelewa wenu wa utambuzi kuhusu kiini cha Mungu bado unahitaji kipindi cha muda mrefu kujifunza, kuthibitisha, kuhisi na kuipitia, hadi siku moja mtajua utakatifu wa Mungu kutoka katikati ya moyo wenu kuwa kiini cha Mungu ambacho hakina dosari, upendo wa Mungu usio na ubinafsi, kwamba haya yote Mungu humpa mwanadamu hayana ubinafsi, na mtakuja kujua ya kwamba utakatifu wa Mungu hauna dosari wala haushutumiki. Hivi viini vya Mungu si maneno tu ambayo Yeye hutumia kuonyesha utambulisho Wake, bali Mungu hutumia kiini Chake kwa kimya na kwa dhati kushughulika na kila mtu. Kwa maneno mengine, kiini cha Mungu si tupu, wala si cha nadharia au mafundisho ya dini na hakika si aina ya maarifa. Si aina ya elimu kwa mwanadamu, lakini badala yake ni ufunuo wa kweli wa matendo ya Mungu mwenyewe na ni kiini ambacho kimefichuliwa cha kile Mungu anacho na alichio. Binadamu anapaswa kujua kiini hiki na kukifahamu, kwa kuwa kila kitu Mungu hufanya na kila neno Yeye husema ni la thamani kubwa na umuhimu mkubwa kwa kila mtu. Unapokuja kuelewa utakatifu wa Mungu, basi unaweza kweli kumwamini Mungu; unapokuja kuelewa utakatifu wa Mungu, basi unaweza kweli kutambua maana halisi ya maneno haya “Mungu Mwenyewe, wa Kipekee.” Hatafikiria tena kwamba unaweza kuchagua kutembea njia zingine, na hutakuwa tena radhi kusaliti kila kitu ambacho Mungu amekupangia. Kwa sababu kiini cha Mungu ni takatifu, hiyo ina maana kwamba kupitia tu Mungu ndipo unaweza kutembea njia yenye kung’aa na sahihi katika maisha; ni kupitia tu Mungu unaweza kujua maana ya maisha, ni tu kupitia Mungu unaweza kuishi kwa kudhihirisha ubinadamu halisi, kumiliki ukweli, kujua ukweli, na ni kupitia tu Mungu unaweza kupata maisha kutoka kwa kweli. Ni Mungu Mwenyewe tu anaweza kukusaidia kuepuka maovu na kukuokoa kutoka kwa madhara na udhibiti wa Shetani. Kando na Mungu, hakuna mtu au kitu kinaweza kukuokoa kutoka kwa bahari ya mateso, ili usiteseke tena: Hili linaamuliwa na kiini cha Mungu. Ni Mungu Mwenyewe tu hukuokoa bila ubinafsi wowote, ni Mungu pekee anayehusika na maisha yako ya baadaye, na hatima yako na maisha yako, na Yeye anapanga mambo yote kwa ajili yako. Hili ni jambo ambalo hakuna kitu ambacho kimeumbwa au hakijaumbwa kinaweza kutimiza. Kwa sababu hakuna kitu ambacho kimeumbwa au hakijaumbwa kina kiini cha Mungu kama hiki, hakuna mtu au kitu kina uwezo wa kukuokoa au kukuongoza wewe. Huu ndio umuhimu wa kiini cha Mungu

kwa mwanadamu. Labda mnahisi kuwa maneno haya Niliyoyasema yanaweza kweli kusaidia kimsingi katika kanuni. Lakini kama wewe unafuatilia ukweli, kama wewe unapenda ukweli, katika uzoefu wako wa baada ya hapa maneno haya hayataleta tu mabadiliko katika hatima yako, lakini zaidi ya hayo yatakuleta kwa njia sahihi ya maisha. Je, unafahamu hili, siyo? (Ndiyo.) Kwa hivyo sasa mna moyo wa kupenda katika kujua kiini cha Mungu? (Ndiyo.) Ni vizuri kuwa na moyo wa kupenda. Tutamalizia hapa kujadili mada yetu ya leo juu ya kujua utakatifu wa Mungu.

Ningependa kuwazungumzia kuhusu kitu mlichofanya kilichonishangaza mwanzoni mwa mkusanyiko wetu leo. Wengine wenu pengine mlikuwa na hisia za shukrani hivi karibuni, ama kuhisi shukrani, na hivyo mlitaka kuonyesha kimwili kile mlichokuwa nacho akilini mwenu. Hili si la kushutumiwa, na si sahihi wala makosa. Lakini ningependa muelewe kitu. Ni nini hiki? Kwanza Ningetaka kuwauliza kuhusu mlichokifanya hivi sasa. Je, kulikuwa ni kusujudu ama kupiga magoti kuabudu? Kuna yeyote anayeweza kuniambia? (Tunaamini ilikuwa kusujudu.) Mnaamini kulikuwa kusujudu, kwa hivyo ni nini maana ya kusujudu? (Kuabudu.) Kwa hivyo ni nini kupiga magoti kuabudu basi? Sijashiriki hili na ninyi awali, lakini leo nahisi ni muhimu kushiriki mada hii na ninyi. Je, mnasujudu katika mikusanyiko yenu ya kawaida? (La.) Je, mnasujudu mnaposema sala zenu? (Ndiyo.) Je, mnasujudu kila wakati mnaposema sala zenu, hali zinaporuhusu? (Ndiyo.) Hivyo ni vizuri sana. Lakini kile Ningependa nyinyi muelewe leo ni kwamba Mungu hukubali tu kupiga magoti kwa aina mbili za watu. Hatuhitaji kutafuta maoni katika Biblia ama tabia za watu wa kiroho, na Nitawaambia kitu kweli hapa na sasa. Kwanza, kusujudu na kupiga magoti kuabudu si kitu sawa. Mbona Mungu anakubali kupiga magoti kwa wale wanaosujudu wenyewe? Ni kwa sababu Mungu humwita mtu Kwake na humwita mtu huyu kukubali agizo la Mungu, kwa hivyo anasujudu mwenyewe mbele ya Mungu. Huyu ni mtu wa aina ya kwanza. Aina ya pili ni kupiga magoti kuabudu kwa mtu anayemcha Mungu na kuepukana na maovu. Kuna watu hawa wa aina mbili tu. Kwa hivyo mko katika aina gani? Mnaweza kusema? Huu ni ukweli kabisa, ingawa unaweza kuumiza hisia zenu kidogo. Hakuna kitu cha kusema kuhusu kupiga magoti kwa watu wakati wa sala—hii ni sahihi na ndivyo inavyopaswa kuwa, kwa sababu wakati watu wanasali wakati mwingi ni kuombea kitu, kufungua mioyo yao kwa Mungu na kukutana Naye uso kwa uso. Ni mawasiliano na mazungumzo, moyo kwa moyo na Mungu. Mkiifanya kama urasmi tu, basi haipaswi kufanya hivyo. Simaanishi kuwashutumu kwa yale ambayo mmefanya leo. Mnajua kwamba nataka tu kuweka wazi kwenu ili muelewe kanuni hii, mnajua? (Tunajua.) Ili msiendelee kufanya hili. Je, watu basi wana fursa yoyote ya kusujudu na kupiga magoti mbele ya uso wa Mungu? Daima kutakuwa na fursa. Hatimaye siku itakuja lakini wakati sio sasa. Mnaona? Je, hili linawafanya kuhisi vibaya? (La.) Hivyo ni vizuri. Labda maneno haya yatawatia moyo ama kuwashawishi ili muweze kujua katika

mioyo yenu taabu ya sasa kati ya Mungu na mwanadamu na aina ya uhusiano uliopo sasa kati yao. Ingawa tumeongea na kuzungumza sana hivi karibuni, uelewa wa mwanadamu kuhusu Mungu bado uko mbali na kutosha. Mwanadamu bado ana umbali mrefu wa kwenda katika njia hii ya kutafuta kumwelewa Mungu. Si nia yangu kuwafanya mfanye hivi kwa dharura, ama kuwaharakisha kuonyesha matamania na hisia za aina hizi. Yale mliyofanya leo yanaweza kufichua na kuonyesha hisia zenu za kweli, na Niliyafahamu. Kwa hivyo wakati mlipokuwa mkiyafanya, nilitaka tu kusimama na kuwatakiya mema, kwa sababu Nataka nyote muwe wazima. Kwa hivyo katika maneno na vitendo vyangu vyote ninafanya yote ninayoweza kuwasaidia, kuwaongoza, ili muwe na uelewa sahihi na mtazamo sahihi wa mambo yote. Mnaweza kuelewa haya, sivyo? (Ndiyo.) Hivyo ni vizuri sana. Ingawa watu wana baadhi ya uelewa wa tabia mbalimbali za Mungu, kipengele cha kile anacho Mungu na alichio na kazi Mungu anafanya, wingi wa uelewa huu hauendi mbali na kusoma maneno kwenye ukurasa, ama kuyaelewa katika kanuni, ama tu kuyafikiria. Yale wanayoyakosa sana watu ni uelewa na mtazamo wa kweli unaotoka kwa uzoefu halisi. Ingawa Mungu hutumia njia mbalimbali kuamsha mioyo ya wanadamu, bado kuna njia ndefu ya kutembea kabla mioyo ya wanadamu iamshwe kikamilifu. Sitaki kumwona yeyote akihisi kana kwamba Mungu amemwacha nje kwa baridi, kwamba Mungu amemwacha ama amempuuza. Ningetaka tu kuona kila mtu katika njia ya kufuatilia ukweli na kutafuta kumwelewa Mungu, akiendelea mbele kwa ujasiri na utashi usiosita, bila wasiwasi, bila kubeba mizigo. Haijalishi umefanya makosa gani, haijalishi umepotoka aje ama vile ulivyotenda dhambi, usiwache haya yawe mizigo ama vikorokoro ziada kubeba katika ufuataji wako wa kumwelewa Mungu: Endelea kutembea mbele. Nyakati zote, Mungu hushikilia wokovu wa mwanadamu moyoni Mwake; hili halibadiliki kamwe. Hii ni sehemu ya thamani sana ya kiini cha Mungu. Mnahisi vizuri kiasi sasa? (Ndiyo.) Ninatumai kwamba mnaweza kuchukua mtazamo sahihi katika mambo yote na maneno ambayo Nimezungumza. Wacha tukomeshe ushirika wetu hapa, basi. Kwaheri kila mtu! (Kwaheri!)

Januari 11, 2014

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee VII

Mhutasari wa Mamlaka ya Mungu, Tabia ya Haki ya Mungu, na Utakatifu wa Mungu

Mnapomaliza maombi yenu, je, mioyo yenu inahisi utulivu katika uwepo wa Mungu? (Ndiyo.) Ikiwa moyo wa mtu unaweza kutulizwa, ataweza kusikia na kuelewa neno la Mungu na

ataweza kusikia na kuuelewa ukweli. Ikiwa moyo wako hauwezi kutulizwa, ikiwa moyo wako siku zote unayoyoma, au siku zote unafikiria juu ya mambo mengine, utaathiri kuja kwako pamoja kusikia neno la Mungu. Sasa, ni kitu gani cha msingi tunachokijadili wakati huu? Hebu sote turudi nyuma kidogo katika hoja kuu. Kuhusiana na kumjua Mungu Mwenyewe, yule wa kipekee, katika sehemu ya kwanza, tulijadili mamlaka ya Mungu. Katika sehemu ya pili, tulijadili tabia ya haki ya Mungu. Na tulijadili utakatifu wa Mungu katika sehemu ya tatu. Maudhui mahususi tuliyojadili kila mara yamewacha wazo kwako? Katika sehemu ya kwanza “mamlaka ya Mungu,” kitu kipi kimeacha wazo la kina sana kwako, ni sehemu gani imekuwa na matokeo makubwa kwako? (Mungu kwanza alizungumza juu ya mamlaka na nguvu ya neno la Mungu; Mungu ni mwema kama neno Lake na neno Lake litakuwa kweli. Hiki ndicho kiini cha asili cha Mungu.) (Maagizo ya Mungu kwa Shetani kwamba anaweza kumjaribu Ayubu, lakini hawezi kuchukua uhai wake. Kutokana na hili tunayaona mamlaka ya neno la Mungu.) Je, kuna kitu kingine cha kuongeza? (Mungu alitumia maneno kuumba mbingu na nchi na vitu vyote ndani yake, na anazungumza kuweka agano na mwanadamu na kuweka baraka Zake juu ya mwanadamu. Hii yote ni mifano ya mamlaka ya neno la Mungu. Kando na hayo, tunaona pale ambapo Bwana Yesu alimwamuru Lazaro kutoka kaburini kwamba uhai na kifo vipo chini ya udhibiti wa Mungu, ambavyo Shetani hana uwezo wa kudhibiti na kwamba haijalishi kazi ya Mungu inafanyika katika mwili au katika Roho, mamlaka Yake ni ya pekee.) Huu ni uelewa mlioupata baada ya kusikia ushiriki, sio? Tunapozungumza kuhusu mamlaka ya Mungu, mnaelewa nini kuhusu neno “mamlaka”? Ndani ya mawanda ya mamlaka ya Mungu, katika kile ambacho Mungu anafanya na kufichua, watu wanaona nini? (Tunaona ukuu na hekima ya Mungu.) (Tunaona kwamba mamlaka ya Mungu yapo siku zote na kwamba kweli, kweli yapo. Tunayaona mamlaka ya Mungu kwa upana kwenye utawala Wake juu ya mbingu, na tunayaona kwa ufinyu kadri anavyodhibiti maisha ya binadamu. Mungu kweli anapanga na kudhibiti awamu zile sita za maisha. Aidha, tunaona kwamba mamlaka ya Mungu yanamwakilisha Mungu Mwenyewe, yule wa kipekee, na hakuna viumbe vilivyoumbwa au ambavyo havijaumbwa vinaweza kuwa nayo. Mamlaka ya Mungu ni alama ya hadhi Yake.) “Alama za hadhi ya Mungu na nafasi ya Mungu,” mnaonekana kuwa na uelewa wa kimafundisho wa maneno haya. Je, mna ufahamu wowote wa maana kuhusu mamlaka ya Mungu? (Mungu ametuangalia na kutulinda tangu tukiwa wadogo, na tunayaona mamlaka ya Mungu katika hilo. Hatukujua kuhusu hatari zilizotupata, lakini Mungu siku zote alikuwa anatulinda kisiri; haya pia ni mamlaka ya Mungu.) Vizuri sana, imesemwa vyema.

Tunapozungumza kuhusu mamlaka ya Mungu, mkazo upo wapi, hoja kuu? Kwa nini tunahitaji kujadili maudhui haya? Kwanza, madhumuni ya kujadili maudhui haya ni kwa watu kuthibitisha hadhi ya Mungu kama Muumba na nafasi Yake miongoni mwa vitu vyote; hili ni

jambo wanaweza kuelewa, jambo wanaloweza kuona na kuhisi. Kile unachokiona na kukihisi yote yanatokana na matendo ya Mungu, maneno ya Mungu na udhibiti wa Mungu wa ulimwengu. Hivyo, watu hupata ufahamu upi wa kweli kupitia yote wanayoona, kujifunza, na kujua kupitia mamlaka ya Mungu? Hili ndilo jambo la kwanza, ambalo tayari tumejadili. Pili, watu wanapoona yote ambayo Mungu amefanya na kusema na kuyadhibiti kupitia mamlaka Yake. Ni ili kukuruhusu uone jinsi Mungu alivyo mwenye nguvu na mwenye hekima katika kudhibiti Kwake kila kitu. Je, hili halikuwa lengo na hoja kuu ya mazungumzo yetu ya awali ya mamlaka ya pekee ya Mungu? Sio muda mrefu umepita na baadhi ya watu tayari wameshasahau hili, kitu kinachothibitisha kwamba hamjapata ufahamu wa kina wa mamlaka ya Mungu. Inaweza hata kusemwa kwamba mwanadamu hajayaona mamlaka ya Mungu. Sasa mnaelewa hili angalau kidogo? Unapoyaona mamlaka ya Mungu katika vitendo, utahisi nini hasa? Mmehisi kweli nguvu ya Mungu? (Tumehisi.) Unaposoma maneno ya Mungu kuhusu uumbaji Wake wa ulimwengu unahisi nguvu Yake, unauhisi uweza Wake. Unapoona utawala wa Mungu juu ya hatima ya wanadamu, unahisi nini? Je, unahisi nguvu Yake na hekima Yake? Ikiwa Mungu hakuwa na nguvu hii, ikiwa hakuwa na hekima hii, je, Angekuwa na sifa za kutawala vitu vyote na juu ya hatima ya wanadamu? Mungu ana nguvu na hekima, na hivyo Ana mamlaka. Hili ni jambo la kipekee. Je, umewahi kumjua kiumbe yeyote au mtu ulimwenguni ambaye ana nguvu kama alizonazo Mungu? Je, kuna mtu yeyote au kitu chochote chenye nguvu za kuumba mbingu na nchi na vitu vyote vile vile kuvithibiti na kuvitawala? Je, kuna mtu yeyote au kitu chochote kinachoweza kutawala na kuwaongoza wanadamu wote na kuwapo siku zote na chenye uweza? (Hapana, hakuna.) Sasa unaelewa maana ya kweli ya yale yote yaliyomo katika mamlaka ya kipekee ya Mungu? Je, mna uelewa kiasi fulani? (Ndio, tunao.) Sasa tumemaliza kupitia hoja za mamlaka ya Mungu ya kipekee.

Katika sehemu ya pili, tulizungumza kuhusu tabia ya haki ya Mungu. Hatukujadili mambo mengi kuhusu tabia ya haki ya Mungu. Hii ni kwa sababu kazi ya Mungu katika hatua hii kimsingi ni ya hukumu na kuadibu. Tabia ya haki ya Mungu imefichuliwa wazi katika Enzi ya Ufalme, kwa umahususi kabisa. Amesema maneno ambayo hajawahi kuyasema kutoka wakati wa uumbaji; na katika maneno Yake watu wote, wote ambao wameliona neno Lake, na wote ambao wamepitia uzoefu wa neno Lake wameiona tabia Yake ya haki ikifichuliwa. Sasa hoja kuu ya kile tunachokijadili kuhusu tabia ya haki ya Mungu ni nini? Je, mmekuza ufahamu wa kina wa kile ambacho mmejifunza? Je, mmepata uelewa kutokana na uzoefu wenu wowote? (Mungu kuiteketeza Sodoma kwa moto ilikuwa ni kwa sababu watu wa wakati huo walikuwa waovu sana na hivyo wakaichochea ghadhabu ya Mungu. Ni kutokana na hili ndipo tunaiona tabia ya haki ya Mungu.) Kwanza, hebu tuangalie: Ikiwa Mungu asingeiangamiza Sodoma, je, ungeweza kuijua tabia Yake ya haki? Bado ungeweza kujua, siyo? Unaweza kuiona kupitia

maneno Aliyoyaeleza katika Enzi ya Ufalme, na pia kwa hukumu Yake, kuadibu, na laana zilizotolewa dhidi ya mwanadamu. Je, mnaiona tabia ya haki ya Mungu kwa kuacha kuiangamiza Ninawi? (Ndiyo.) Katika enzi ya sasa, watu wanaweza kuona rehema, upendo na uvumilivu kiasi wa Mungu, na watu wanaweza pia kuiona mabadiliko ya moyo wa Mungu yanayofuata toa ya mwanadamu. Baada ya kutoa mifano hii miwili kuanzisha mjadala wetu wa tabia ya haki ya Mungu, iko wazi kabisa kuona kwamba tabia Yake ya haki imefichuliwa. Hata hivyo, katika uhalisia hii haiko tu kwa kile kilichorekodiwa katika visa viwili hivi vya Biblia. Kutokana na kile sasa umejifunza na kuona kupitia neno la Mungu na kazi Yake, kutokana na uzoefu wako wa sasa juu yao, tabia ya haki ya Mungu ni nini? Jadili kutokana na uzoefu wako binafsi. (Katika mazingira ambayo Mungu aliwatengenezea watu, pale wanapoweza kuutafuta ukweli na kutenda chini ya mapenzi ya Mungu, Mungu huwaongoza, huwapa nuru, na kuwafanywa wahisi mwangaza ndani yao. Watu wanapokwenda kinyume cha Mungu na kumpinga na kwenda kinyume cha mapenzi Yake, kunakuwa na giza ndani yao, kana kwamba Mungu amewatelekeza. Hata wanaomba lakini hawajui nini cha kumwambia, lakini pale ambapo wanaweka pembeni mawazo yao na kuweka pembeni dhana zao na kuwa tayari kushirikiana na Mungu na kujitahidi kujiboresha, ni hapa ndipo uso wa tabasamu wa Mungu unaanza kuonekana taratibu. Kutoka kwa hili tumepitia utakatifu wa tabia ya haki ya Mungu; Mungu huonekana katika ufalme mtakatifu na anafichika mahali penye uchafu.) (Ninaiona tabia ya haki ya Mungu kwa vile anavyowachukulia watu. Kaka zetu na dada zetu wanatofautiana katika kimo na ubora wa tabia, na kile ambacho Mungu anakitaka kutoka kwa kila mmoja wetu hutofautiana vile vile. Wote tunaweza kupokea nuru ya Mungu kwa viwango tofauti, na kwa namna hii ninaiona haki ya Mungu. Hii ni kwa sababu mwanadamu hawezi kumtendea mwanadamu kwa namna hii hii, ni Mungu pekee ndiye anaweza kufanya hivyo.) Nyote mmeongea maarifa ya kiutendaji.

Je, unaelewa hoja kuu kuhusu kuifahamu tabia ya haki ya Mungu? Kuna mengi yanayoweza kusemwa kutokana na uzoefu juu ya mada hii, lakini kwana kuna hoja chache ambazo lazima Niwaambie. Kuielewa tabia ya haki ya Mungu, kwanza mtu anapaswa kuelewa hisia za Mungu: kile Anachokichukia, kile Anachokichukia kabisa, kile Anachokipenda, ni mvumilivu na mwenye huruma kwa nani, na ni aina gani ya mtu anayepokea rehema hiyo. Hii ni hoja ya msingi kufahamu. Aidha, mtu anapaswa kuelewa kwamba haijalishi Mungu ni mwenye upendo kiasi gani, haijalishi ni Mwenye rehema na upendo kiasi gani kwa watu, Mungu hamvumilii mtu yeyote anayekosea hali na nafasi Yake, wala Hamvumilii mtu yeyote anayekosea heshima Yake. Ingawa Mungu anawapenda watu, Hawadekezi. Anawapatia watu upendo Wake, rehema Yake, na uvumilivu Wake, lakini hajawahi kuwakuwadia; Ana kanuni Zake na mipaka Yake. Bila kujali ni kwa kiwango gani umeuhisi upendo wa Mungu ndani yako, bila kujali upendo huo ni wa kina kiasi gani, hupaswi kamwe kumtendea Mungu kama ambavyo

ungemtendea mtu mwingine. Ingawa ni kweli kwamba Mungu anawachukulia watu kama wako karibu Naye, ikiwa mtu anamwanguka Mungu kama mtu mwingine, kana kwamba ni kiumbe mwingine wa uumbaji, kama rafiki au kama kitu cha kuabudu, Mungu atawaficha uso Wake na kuwatelekeza. Hii ndiyo tabia Yake, na watu hawapaswi kulichukulia jambo hili kwa mzaha. Hivyo, mara nyingi sisi huona maneno kama haya yकिननwa na Mungu kuhusu tabia Yake: Haijalishi umesafiri njia nyingi kiasi gani, umefanya kazi kubwa kiasi gani au umevumilia kiasi gani, mara tu unapoikosea tabia ya Mungu, Atamlipa kila mmoja wenu kulingana na kile ulichokifanya. Hii ina maana kwamba Mungu huwaona watu kama wapo karibu na Yeye, lakini watu hawapaswi kumchukulia Mungu kama rafiki au ndugu. Usimchukulie Mungu kama rafiki yako. Haijalishi ni upendo kiasi gani umepokea kutoka Kwake, haijalishi Amekuvumilia kwa kiasi gani, hupaswi kabisa kumchukulia Mungu kama rafiki tu. Hii ndiyo tabia ya haki ya Mungu. Uaelewa, sio? Je, kuna haja ya Mimi kusema zaidi kuhusu hili? Je, una uelewa wowote wa awali kuhusiana na suala hili? Kwa ujumla, hili ndilo kosa rahisi sana ambalo watu wanafanya bila kujali kama wanaelewa mafundisho, au kama hawajafikiria chochote kuyahusu hapo awali. Watu wanapomkosea Mungu, inaweza isiwe kwa tukio moja, au kitu kimoja walichokisema, bali ni kwa sababu ya mtazamo walionao na hali waliyomo. Hili ni jambo la kutisha sana. Baadhi ya watu wanaamini kwamba wana uelewa juu ya Mungu, kwamba wanamjua, hata wanaweza kufanya baadhi ya mambo ambayo yanaweza kumpendeza Mungu. Wanaanza kuhisi wako sawa na Mungu na kwamba kwa werevu wamekuwa na urafiki na Mungu. Aina hizi za hisia sio sahihi kabisa. Ikiwa huna uelewa wa kina juu ya hili, ikiwa huelewi vizuri hili, basi ni rahisi sana kumkosea Mungu na kukosea tabia Yake ya haki. Unaelewa hili sasa, siyo? Je, tabia ya haki ya Mungu sio ya kipekee? Je inaweza kamwe kuwa sawa na tabia ama maadili ya mwanadamu? Haiwezi kamwe. Hivyo, hupaswi kusahau kwamba haijalishi ni kwa namna gani Mungu anawachukulia watu, haijalishi ni namna gani Anafikiri juu ya watu, nafasi, tabia na hadhi ya Mungu kamwe havibadiliki. Kwa binadamu, Mungu siku zote ni Bwana wa vitu vyote na Muumbaji.

Umejifunza nini kuhusu utakatifu wa Mungu? Katika sehemu hiyo kuhusu “utakatifu wa Mungu,” kando na ukweli kwamba uovu wa Shetani unatumika kama foil^[a], maudhui makuu ya mjadala wetu kuhusu utakatifu wa Mungu yalikuwa yapi? Je, sio kile ambacho Mungu anacho na alichu? Je, kile ambacho Mungu anacho na alichu ni vya kipekee kwa Mungu Mwenyewe? (Ndiyo.) Hakuna chochote katika viumbe vyake kina hii. Hivyo tunasema kwamba utakatifu wa Mungu ni wa kipekee. Hiki ni kitu ambacho unaweza kuelewa. Tulikuwa na mikutano mitatu juu ya utakatifu wa Mungu. Unaweza kufafanua kwa maneno yako mwenyewe, kwa uelewa wako mwenyewe, kile unachoamini ni utakatifu wa Mungu? (Mara ya mwisho ambapo Mungu aliwasiliana na sisi tulisujudu mbele Yake. Mungu aliwasiliana na sisi ukweli kuhusu kusujudu

na kuinama kumwabudu, Tuliona kwamba haikuwa kulingana na mapenzi Yake kwamba tuliinama na kumwabudu wakati hatukuwa tumefikia matakwa Yake, na kutoka hili tuliona utakatifu wa Mungu.) Kweli kabisa, sio? Je, kuna kitu chochote kingine? (Katika neno la Mungu kwa mwanadamu, tunaona kwamba Anazungumza kwa wazi na kwa kueleweka, Analenga moja kwa moja kwenye hoja ya msingi. Shetani anazungumza kwa kuzungukazunguka na ni mwenye uongo mwingi. Kutokana na kile kilichotokea wakati uliopita wakati tuliposujudu kifudufudi mbele ya Mungu, tuliona kwamba maneno Yake na matendo Yake siku zote yanaongozwa na kanuni. Siku zote yupo wazi na wa kueleweka Anapotuambia jinsi gani tunavyopaswa kutenda, tunachopaswa kushikamana nacho, na jinsi gani tunavyopaswa kuchukua hatua. Lakini watu hawapo hivi; baada ya binadamu kuharibiwa na Shetani, watu walitafuta kufikia matakwa na nia zao binafsi, na tamaa zao binafsi katika matendo na maneno yao. Kutokana na namna ambayo Mungu anamwangalia binadamu, kutokana na uangalizi na ulinzi Anaowapatia, tunaona kwamba yote ambayo Mungu anafanya ni mazuri, na yako wazi kabisa. Ni kwa namna hii ndipo tunaona ufunuo wa kiini cha utakatifu wa Mungu.) Imesemwa vizuri! Je, kuna mtu yeyote aliye na jambo la kuongezea? (Kupitia kwa Mungu kufunua kiini kiovu cha Shetani, tunauona utakatifu wa Mungu, tunapata ufahamu zaidi wa wa uovu wa Shetani, na kuona chanzo cha mateso yote ya mwanadamu. Hapo nyuma, tulikuwa hatuna habari ya mateso chini ya utawala wa Shetani. Ni baada tu ya Mungu kufichua hili ndipo tuliona kwamba mateso yote yanayotokana na kufuatilia umaarufu na utajiri ni kazi ya Shetani. Ni hapo tu ndipo tulihisi kwamba utakatifu wa Mungu ndio wokovu wa kweli wa binadamu.) Kuna kitu chochote cha kuongezea hapo? (Watu wapotovu hawana maarifa ya kweli au upendo kwa Mungu. Kwa sababu hatuelewi kiini cha utakatifu wa Mungu, kuinama kwetu mbele Yake katika ibada kumeghushiwa, kuna makusudi yaliyofichika na kwa kukusudia, kitu kinachomfanya Mungu asiwe na furaha. Tunauona kwamba Mungu yupo tofauti sana na Shetani; Shetani anawataka watu kumsujudia na kujipendekeza kwake, kumwinamia na kumwabudu. Shetani hana kanuni. Kutokana na hili natambua utakatifu wa Mungu.) Vizuri sana! Kutokana na kile tulichoshiriki kuhusu utakatifu wa Mungu, je, mmeuona ukamilifu wa Mungu? (Tumeuona.) Je, mnaona jinsi ambavyo Mungu ni chanzo cha mambo yote mazuri? Je, mnaweza kuona jinsi ambavyo Mungu ni mfano halisi wa ukweli na haki? Je, mnaona jinsi ambavyo Mungu ni chanzo cha upendo? Je, mnaona jinsi ambavyo yote ambayo Mungu anayafanya, yote ambayo anayatoa, na yote ambayo Anayafichua hayana makosa? (Tunaona hili.) Mifano hii kadhaa yote ni hoja kuu kuhusu utakatifu wa Mungu ambao Nauzungumzia kuhusu. Leo, maneno haya yanaweza kuonekana kama mafundisho tu kwako, lakini siku moja, utakapopita uzoefu na kumshuhudia Mungu wa kweli Mwenyewe kutoka katika neno Lake na kazi Yake, utasema kwa dhati kwamba Mungu ni mtakatifu, kwamba Mungu ni tofauti na binadamu, na kwamba moyo Wake, tabia Yake, na asili yote ni takatifu. Utakatifu huu unamruhusu mwanadamu kuuona ukamilifu Wake na vile vile humfanya

mwanadamu kuona kwamba asili ya utakatifu wa Mungu haina mawaa. Asili ya utakatifu wake inaamua kwamba Yeye ni Mungu Mwenyewe wa kipekee, na inamwonyesha mwanadamu, na kuthibitisha kwamba ni Mungu Mwenyewe wa kipekee. Je, hii si hoja kuu? (Ni hoja kuu.)

Leo tumefanya muhtasari wa sehemu kadhaa za maudhui kutoka katika mikutano iliyotangulia. Tutakamilisha muhtasari wetu hapa. Ni matumaini yangu kuwa kila mmoja wenu ataweka moyoni hoja kuu za kila kipengele na mada. Usizifikirie tu kuwa ni mafundisho; zisome zote na jaribu kuzitafakari pale unapopata muda. Zikumbuke katika nyoyo zenu na mziweke katika uhalisi—kisha hakika utapitia yote ambayo Nimesema kuhusu uhalisi wa Mungu kufichua tabia Yake na kufichua kile Anacho na alichio. Hata hivyo hutaweza kuzielewa ikiwa utaziandika tu katika kitabu chako bila kuzisoma zote au kuzifikiria tena. Unaelewa, siyo? Baada ya kuviwasilisha vipengele hivi vitatu, watu watakuwa wamepata uelewa wa jumla au hata mahususi juu ya hadhi ya Mungu, asili Yake, na tabia Yake. Je, watakuwa na uelewa kamili juu ya Mungu lakini? (La.) Sasa, katika uelewa wenu binafsi juu ya Mungu, je, kuna maeneo mengine ambapo mnahisi mnahitaji uelewa wa kina? Hiyo ni kusema, baada ya kuwa umepata uelewa wa mamlaka ya Mungu, tabia Yake ya haki, na utakatifu Wake, pengine umeyakinisha katika akili yako mwenyewe utambuzi wa hadhi na nafasi Yake ya kipekee, lakini kupitia uzoefu wako unapaswa kufahamu na kutambua matendo Yake, uwezo Wake, na asili Yake kabla ya kuweza kupata uelewa wa kina. Sasa mmesikiliza ushirika huu hivyo mnaweza kuweka moyoni mwako makala haya ya imani: Mungu kweli yupo na ni ukweli kwamba Anaendesha vitu vyote. Hakuna mwanadamu anayepaswa kuikosea tabia Yake ya haki na utakatifu Wake ni hakika kiasi kwamba mwanadamu hawezi kuushuku. Huu ni ukweli. Ushirika huu unafanya hadhi na nafasi ya Mungu kuwa na msingi katika mioyo ya watu. Punde msingi huu kuanzishwa, watu lazima wajaribu kuelewa zaidi.

Mungu ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote (I)

Leo Nitashiriki nawe mada mpya. Mada itakuwa ni nini? Kichwa cha mada kitakuwa “Mungu ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote.” Je, hii siyo mada kubwa kidogo kuweza kuijadili? Je, inaonekana kama kitu ambacho kidogo hakiwezi kufikika? Mungu kuwa chanzo cha uhai kwa vitu vyote inaweza kuonekana ni mada ambayo watu wanahisi kutohusika nayo, lakini wote wanaomfuata Mungu wanapaswa kuielewa. Hii ni kwa sababu mada hii haihusiani kwa kuchanganulika na kila mtu anayemjua Mungu, kuweza kumridhisha na kumheshimu. Hivyo, mada hii inapaswa kuwasilishwa. Awali, pengine baadhi ya watu walikuwa na ufahamu wa msingi wa mada hii, au pengine baadhi ya watu waliifahamu. Wanaweza wakawa na ufahamu sahili kuhusu au ufahamu wa juu juu wa hii katika akili zao. Wengine wanaweza kuwa na ufahamu kiasi maalumu kuihusu; kutokana na uzoefu wao wa kipekee, mioyoni mwao wana

uelewa wa kina juu ya mada hii. Lakini ama maarifa ya mada hii ni ya kina au ya juujuu, kwenu nyinyi ni ya upande mmoja na wala si mahususi vya kutosha. Hivyo, mada hii inapaswa kuwasilishwa, kusudi lake ni kuwapatia uelewa wa kina zaidi na mahususi. Nitatumia njia maalumu kushiriki na nyinyi mada hii, njia ambayo hatujawahi kuitumia hapo awali na njia ambayo kidogo mtaona si ya kawaida, au ambayo haifurahishi kidogo. Hata hivyo, baada ya kuisikia mtaijua, njia yoyote ile itakayotumika. Je, mnapenda kusikiliza hadithi? (Ndiyo.) Inaonekana kwamba Nilikuwa sahihi kuchagua njia ya kusimulia hadithi. Nyinyi nyote mnapenda kusikiliza hadithi. Sawa, hebu tuanze. Hamna haja ya kuandika hii kwenye matini zenu. Ninawaomba muwe watulivu, na msihangaike. Unaweza kufumba macho yako ikiwa unahisi kwamba kufumbua macho yako mazingira yanayokuzunguka au watu wanaokuzunguka wanaweza kukupotezea umakini. Nina hadithi ndogo nzuri ya kuwasimulia. Ni hadithi kuhusu mbegu, ardhi, mti, mwanga wa jua, chiriku, na mwanadamu. Hadithi Ninayokwenda kuwasimulia ina wahusika gani wakuu ndani yake? (Mbegu, ardhi, mti, mwanga wa jua, chiriku, na mwanadamu.) Mungu atakuwa ndani yake? (Hapana.) Lakini Nina uhakika kwamba baada ya hadithi kusimuliwa mtajihisi kuburudika na kuridhika. Sawa basi, unaweza kusikiliza kimya kimya.

Hadithi ya 1. Mbegu, Ardhi, Mti, Mwanga wa Jua, Chiriku, na Mwanadamu

Mbegu ndogo ilidondoka ardhini. Baada ya mvua kubwa kunyesha, mbegu ilianza kuchipuka na mizizi yake ikamea taratibu kwenda ardhini. Chipuko lilirefuka kadri muda ulivyozidi kwenda, yakivumilia upepo mkali na mvua kubwa, yakiangalia mabadiliko ya misimu kadri mwezi unavyopevuka na kufifia. Wakati wa kiangazi ardhi ilileta zawadi ya maji ili kwamba chipuko liweze kuhimili joto kali. Na kwa sababu ya ardhi, chipuko halikuhisi joto na hivyo lilihimili joto la kiangazi. Msimu wa baridi ulipokuja, ardhi ililifunika chipuko katika kumbatio la vuguvugu lake na kushikamana kwa nguvu. Na kwa sababu ya vuguvugu la ardhi, chipuko lilihimili baridi kali, likivuka bila kudhurika katika dhoruba ya msimu wa baridi na barafu za msimu. Likivikwa na ardhi, chipuko lilikua kwa ujasiri na lilikuwa na furaha. Lilirefuka na kujivunia malezi yasiyokuwa ya ubinafsi ambayo ardhi iliyatoa. Chipuko lilikua kwa furaha. Liliimba wakati mvua ilipokuwa ikinyesha na kucheza na kuyumba kadri upepo ulivyokuwa ukivuma. Na hivyo, chipuko na ardhi hutegemeana...

Miaka ilipita, na chipuko sasa lilikuwa mnara wa mti. Lilikuza matawi manene juu yake yaliyokuwa na majani yasiyohesabika na kusimama imara juu ya nchi. Mizizi ya mti ilimea aridhini kama ilivyomea hapo kabla, lakini sasa ilizama kabisa ardhini chini kabisa. Kile ambacho mwanzo kilililinda chipuko sasa kilikuwa msingi wa mti mkubwa sana.

Mwale wa mwanga wa jua ulimulika mti na shina likatikisika. Mti ulitoa nje matawi yake

kwa upana na kufaidi sana kutoka kwenye mwanga. Ardhi chini ilipumua kwa wizani pamoja na mti, na ardhi ilihisi kufanywa upya. Baada ya hapo tu, upepo mwanana ulivuma ukitokea katika matawi, na mti ulifurahia sana, ukiwa na nguvu. Na hivyo, mti na mwanga wa jua vinategemeana ...

Watu walikaa katika kivuli tulivu cha mti na wakafurahia hewa changamfu inayonukia vizuri. Hewa ilitakasa mioyo na mapafu yao, na ilitakasa damu ndani yao. Watu hawakuhisi tena kuchoka au kuelemea. Na hivyo, watu na miti wanategemeana ...

Kundi la chiriku waliimba kwa uchangamfu walivyokuwa wakitua kwenye matawi ya mti. Pengine walikuwa wanamwepuka adui fulani, au walikuwa wanazaliana na kuwalea watoto wao, au pengine walikuwa wanapata pumziko fupi. Na hivyo, ndege na mti wanategemeana ...

Mizizi ya mti, ikiwa imesokotana na kusongamana, ilijikita chini kabisa ardhini. Shina lake liliifunika ardhi dhidi ya upepo na mvua na kuyatoa nje matawi yake makubwa na kuilinda ardhi chini yake, na mti ulifanya hivi kwa sababu ardhi ni mama yake. Yanatiana nguvu na kutegemeana, na kamwe hayataachana ...

Na hivyo, hadithi hii imefikia mwisho. Hadithi ambayo Nimewasimulia ilikuwa kuhusu mbegu, ardhi, mti, mwanga wa jua, chiriku na mwanadamu. Hadithi ina sehemu chache tu. Iliwapatia hisia gani? Baada ya kuwasimulia kwa namna hii, je, mmeielewa? (Tunaelewa.) Mnaweza kuzungumza kuhusu hisia zenu. Sasa, Mnahisi nini baada ya kusikia hadithi hii? Kwanza Nitawaambia kwamba vitu vyote Nilivyovitaja kwenu mnaweza kuviona na kuvishika; haya ni mambo halisi, sio sitiari. Ninawataka sasa mtafakari juu ya yale Niliyoyajadili. Hakuna Nilichokizungumza ambacho kilikuwa cha kina, na kuna sentensi chache ambazo zinatengeneza hoja kuu ya hadithi. (Hadithi tuliyoisikia inatoa picha nzuri: Mbegu inapata uhai na kadiri inavyokua inapitia misimu minne ya mwaka: majira ya kuchipua, kiangazi, kipupwe na baridi. Ardhi ni kama mama kwa namna ambavyo inalea. Inatoa vuguvugu wakati wa baridi ili kwamba chipuko lihimili baridi. Baada ya chipuko kukua na kuwa mti, mwale wa jua unagusa matawi yake, ukiupatia mti furaha zaidi. Tunaona kwamba miongoni mwa vitu vyote vya uumbaji wa Mungu, ardhi pia ipo hai na kwamba hiyo na mti vinategemeana. Pia Ninaona joto jingi ambalo jua linaupa mti, na ingawa ndege ni vitu vya kawaida vya kuona, tunaona jinsi gani ndege, mti, na watu wote wanakuja pamoja kwa maafikiano. Tunaposikia hadithi hii, hii ndiyo hisia tuliyonayo mioyoni mwetu kwamba, kimsingi, vitu vyote vya uumbaji wa Mungu ni hai.) Imesemwa vizuri! Je, kuna mtu ana kitu chochote cha kuongeza? (Katika hadithi kadri mbegu inapokua na kuwa mti mrefu kabisa, naona maajabu ya uumbaji wa Mungu. Naonakwamba Mungu alifanya vitu vyote vihimiliane na kutegemeana, na vyote kuunganika pamoja na kuhudumiana. Tunaona hekima ya Mungu, maajabu Yake, na tunaona kwamba Yeye ni chanzo

cha uhai kwa vitu vyote.)

Mambo yote Niliyoyazungumzia ni mambo ambayo mmeshawahi kuyaona hapo awali, kama vile mbegu, mnajua kuhusiana na hili, sio? Mbegu kukua na kuwa mti unaweza usiwe mchakato unaouangalia katika maelezo ya kina, lakini unajua kwamba ni ukweli, sio? Unajua kuhusu ardhi na mwanga wa jua. Taswira ya chiriku wakitua mtini ni kitu ambacho watu wote wamekwishakiona, sio? Na watu kutuliza joto chini ya kivuli cha mti, wote mmekwishawahi kuona, sio? (Tumeona hilo.) Sasa, mnapata hisia gani mnapoona mifano yote hii katika taswira moja? (Upatanifu.) Je, mifano yote hii iliyopo katika taswira hii inatoka kwa Mungu? (Ndiyo.) Kwa kuwa inatoka kwa Mungu, Mungu anajua thamani na umuhimu wa mifano hii kadhaa inayokaa pamoja ardhini. Mungu alipoviumba vitu vyote, Alipofanya mpango na kuumba kila kitu, Alifanya hivyo kwa makusudi; na Alipoumba vitu hivyo, kila kimoja kilijazwa na uzima. Mazingira Aliyotengeneza kwa ajili ya kuwepo binadamu, ambayo yamejadiliwa katika hadithi tuliyoisikia. Imejadili hali ya kutegemeana baina ya mbegu na ardhi; ardhi inastawisha mbegu na mbegu inafungamana na ardhi. Uhusiano kati ya hivi vitu viwili uliamuliwa kabla na Mungu kuanzia mwanzoni kabisa. Mti, mwanga wa jua, chiriku, na mwanadamu katika taswira hii ni mifano ya mazingira hai ambayo Mungu aliyaumba kwa ajili ya mwanadamu. Kwanza, mti hauwezi kuiacha ardhi, wala hauwezi kuishi bila mwanga wa jua. Kwa hivyo, kusudi la Mungu la kuumba mti lilikuwa ni nini? Je, tunaweza kusema kuwa ilikuwa tu ni kwa ajili ya ardhi? Je, tunaweza kusema ilikuwa tu ni kwa ajili ya chiriku? Je, tunaweza kusema ilikuwa tu ni kwa ajili ya watu? (Hapana.) Kuna uhusiano gani kati yao? Uhusiano kati yao ni wa kutiana nguvu, kutegemeana ambapo haviwezi kutengana. Yaani, ardhi, mti, mwanga wa jua, chiriku, na watu wanategemeana kwa ajili ya kuishi na wanaleana. Mti unailinda ardhi wakati ardhi inaulea mti; mwanga wa jua unatoa huduma kwa mti, wakati mti unapata hewa nzuri kutoka katika mwanga wa jua unapunguza joto jingi la mwanga wa jua juu ya ardhi. Nani anayefaidika mwishoni? Mwanadamu ndiye anayefaidika, siyo? Na hii ndiyo kanuni juu ya kwa nini Mungu alifanya mazingira ya kuishi kwa ajili ya binadamu na ambaye ndiye lengo kuu kwa ajili yake. Ingawa hii ni taswira rahisi, tunaweza kuona hekima za Mungu na nia yake. Binadamu hawezi kuishi bila ardhi, au bila miti, au bila chiriku na mwanga wa jua, sio? Ingawa ilikuwa ni hadithi, kile inachoonyesha ni mfano mdogo wa uumbaji wa Mungu wa mbingu na dunia na vitu vyote na zawadi Yake ya mazingira ambamo binadamu wanaweza kuishi.

Mungu aliumba mbingu na nchi na vitu vyote kwa ajili ya mwanadamu na pia akafanya mazingira ya kuishi. Kwanza, hoja kuu tuliyoijadili katika hadithi ni mwingiliano wa mahusiano na hali ya kutegemeana ya vitu vyote. Chini ya kanuni hii, mazingira ya kuishi kwa ajili ya binadamu yamelindwa, yanaendelea kuishi na kudumu; kwa sababu ya uwepo wa mazingira haya hai, mwanadamu anaweza akastawi na kuzaliana. Tuliona mti, ardhi, mwanga wa jua, na

chiriku, na watu katika tukio. Mungu alikuwepo pia? Watu wanaweza wakose kuiona, sio? Lakini mtu aliweza kuona sheria ya kuhimizana na kutegemeana kati ya vitu katika tukio; ni kupitia kanuni hizi ndipo watu wanaweza kuona kwamba Mungu yupo na kwamba ni Mtawala. Mungu anatumia kanuni hizi na sheria kulinda uhai na uwepo wa vitu vyote. Ni kwa njia hii ndipo Anavikimu vitu vyote na Anamkimu binadamu. Je, hadithi hii ina uhusiano wowote na dhamira tuliyoijadili? Kwa juujuu inaonekana kama hakuna uhusiano, lakini kwa uhalisia, kanuni ambazo Mungu anazifanya kama Muumbaji na utawala Wake juu ya vitu vyote zinahusiana kwa karibu sana na Yeye kuwa chanzo cha uhai kwa vitu vyote na zimeunganika bila kuachana. Umejifunza angalau kidogo, sio?

Mungu anaamuru sheria zinazoongoza uendeshaji wa vitu vyote; Anaamuru sheria zinazoongoza uwepo wa vitu vyote; Yeye hudhibiti vitu vyote, na huviweka kutiana nguvu na kutegemeana, ili visiangamie au kutoweka. Hivi tu ndivyo wanadamu wanaweza kuendela kuishi; ni hivyo tu ndivyo wanaweza kuishi chini ya mwongozo wa Mungu katika mazingira kama hayo. Mungu ndiye bwana wa sheria hizi za uendeshaji, na binadamu hawawezi kuingilia na hawawezi kuzibadilisha; ni Mungu Mwenyewe pekee ndiye Anajua kanuni hizi na ni Yeye pekee ndiye anazisimamia. Ni lini miti itachipuka, ni lini mvua itanyesha, ni maji kiasi gani na virutubisho kiasi gani ardhi itaipatia mimea, ni katika msimu gani majani yatapukutika, ni katika msimu gani miti itazaa matunda, jua litaipa miti virutubisho vingapi; kile ambacho miti itatoa nje baada ya kulishwa na jua—vitu hivi vyote viliamuliwa kabla na Mungu alipoumba vitu vyote, kama sheria ambazo hakuna mtu anayeweza kuvunja. Vitu vilivyoundwa na Mungu—ama ni hai au vinaonekana kwa watu si hai—vyote vipo mikononi mwa Mungu na chini ya utawala Wake. Hakuna mtu anayeweza kubadilisha au kuvunja kanuni hii. Hii ni kusema, Mungu alipoviumba vitu vyote Aliweka kanuni ya jinsi vinavyopaswa kuwa. Miti isingeweza kuzamisha mizizi, kuchipua na kukua bila ardhi. Ardhi isingekuwa na miti, ingekauka. Pia, mti ni makazi ya chiriku, ni sehemu ambapo wanapata kujikinga dhidi ya upepo. Je, ingekuwa sawa ikiwa miti ingekuwa bila mwanga wa jua? (Isingekuwa sawa.) Ikiwa miti ingekuwa na ardhi peke yake hiyo isingefanya kazi. Hii yote ni kwa ajili ya mwanadamu na kuendelea kuishi kwa mwanadamu. Mwanadamu anapokea hewa safi kutoka kwenye miti, na anaishi katika ardhi inayomlinda. Mwanadamu hawezi kuishi bila mwanga wa jua, mwanadamu hawezi kuishi bila viumbe hai mbalimbali. Ingawa uhusiano baina ya vitu hivi ni changamani, mnapaswa kukumbuka kwamba Mungu alitengeneza kanuni ambazo zinaongoza vitu vyote ili kwamba viweze kuimarishana, kutegemeana na kuwepo pamoja. Kwa maneno mengine, kila kitu alichokiumba kina thamani na umuhimu. Ikiwa Mungu aliumba kitu bila kuwa na umuhimu, Mungu angeacha kipotee. Hii ni njia mojawapo Aliyoitumia katika kuvikimu vitu vyote. “Kukimu” kuna maana gani katika hadithi hii? Je, Mungu kila siku anatoka na kwenda kumwagilia mti maji? Je, mti unahitaji

msaada wa Mungu ili uweze kupumua? (Hapana.) “Kukimu” hapa ina maana ya usimamizi wa Mungu wa vitu vyote baada ya uumbaji; Alichokuwa akikihitaji kilikuwa ni sheria ili kufanya vitu kwenda vizuri. Mti ulikuwa wenyewe kwa kupandwa ardhini. Masharti ili uweze kukua yote yalitengenezwa na Mungu. Alitengeneza mwanga wa jua, maji, udongo, hewa, na mazingira, upepo, umande, barafu, na mvua, na misimu minne; haya ndiyo masharti ambayo mti huyahitaji ili uweze kukua, hivi ni vitu ambavyo Mungu aliviandaa. Kwa hiyo, Mungu ni chanzo cha mazingira haya hai? (Ndiyo.) Je, Mungu analazimika kwenda kila siku na kuhesabu kila jani kwa miti? Hakuna haja, sio? Mungu pia hahitaji kuusaidia mti ili uweze kupumua. Mungu pia hahitaji kuuamsha mwanga wa jua kila siku kwa kusema, “Ni muda wa kuiangazia miti sasa.” Hana haja ya kufanya hivyo. Mwanga wa jua humulika wenyewe wakati wake wa kumulika unapofika, kulingana na sheria; unaonekana na kumulika juu ya mti na mti unafyonza huo mwanga wakati unapohitaji, na wakati hauhitajiki, mti huo bado huishi ndani ya kanuni. Pengine hamwezi kuelezea jambo hili kwa uwazi, lakini ni ukweli ambao kila mtu anaweza kuona na kuukubali. Chote unachopaswa kufanya ni kutambua kwamba kanuni kwa ajili ya uwepo wa vitu vyote inatoka kwa Mungu na kujua kwamba Mungu ni mkuu juu ya ukuaji na kuishi kwa vitu vyote.

Je, istiari imetumika katika hadithi hii, kama watu wanavyoiita? Je, ni hadithi iliyopewa sifa za kibinadamu? (Hapana.) Kile Nilichokizungumza ni ukweli. Kila kitu ambacho ni hai, kila kitu ambacho kina uhai kipo chini ya utawala wa Mungu. Kilipewa uhai baada ya Mungu kukiumba; ni uhai uliotolewa kutoka kwa Mungu na unafuata sheria na njia Alizozitengeneza kwa ajili yake. Hii haihitaji kubadilishwa na mwanadamu, na haihitaji msaada kutoka kwa mwanadamu; hivi ndivyo Mungu anavyokimu vitu vyote. Unaelewa, sio? Je, unadhani ni lazima watu watambue hili? (Ndiyo.) Hivyo, hadithi hii ina uhusiano wowote na biolojia? Je, inahusiana kwa njia fulani nauwanja wa maarifa au tawi la kujifunza? Hatujadili biolojia hapa na hakika hatufanyi utafiti wa kibiolojia. Je, hoja kuu tunayoizungumzia hapa ni ipi? (Kwamba Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote.) Mnaona nini miongoni mwa vitu vyote vya uumbaji? Mmeiona miti? Mmeiona ardhi? (Ndiyo.) Mmeuona mwanga wa jua, sio? Mmewaona ndege wakikaa mtini? (Ndiyo.) Je, mwanadamu anafurahia kuishi mazingira kama hayo? (Anafurahia.) Yaani, Mungu anatumia vitu vyote—vitu alivyoviumba—kudumisha makazi ya binadamu kwa ajili ya kuishi na kulinda makazi ya binadamu, na hivi ndivyo Anavyomkimu mwanadamu na anavyokimu vitu vyote.

Je, mnappenda mtindo wa hotuba hii, namna Ninavyotoa ushirika? (Ni rahisi kuelewa na kuna mifano ya vitendo ambayo ni halisi.) Hii ni njia ya kweli ya kujadili mambo, sio? Hadithi hii ni ya lazima kuwasaidia watu kutambua kuwa Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote? (Ndiyo.) Kama ni ya lazima, basi tutaendelea na hadithi inayofuata. Maudhui katika hadithi inayofuata ni tofauti kidogo na hoja kuu ni tofauti kidogo pia; mambo yaliyomo katika hadithi

hii ni ambayo watu wanaweza kuona miongoni mwa uumbaji wa Mungu. Sasa, Nitaanza simulizi Yangu ya kufuatia. Tafadhali sikilizeni mkiwa kimya na mwone iwapo mnaweza kuelewa kile Ninachomaanisha. Baada ya kumaliza kusimulia hadithi, nitawauliza maswali kuona mmeelewa kiasi gani. Wahusika wakuu katika hadithi ni mlima mkubwa, kijito kidogo, upepo mkali, na wimbi kubwa.

Hadithi ya 2. Mlima Mkubwa, Kijito Kidogo, Upepo Mkali, na Wimbi Kubwa

Kulikuwa na kijito kidogo kilichotiririka kwa kuzungukazunguka, hatimaye kikawasili chini ya mlima mkubwa. Mlima ulikuwa unazuia njia ya kijito hiki, hivyo kijito kikauomba mlima kwa sauti yake dhaifu na ndogo, “Tafadhali naomba kupita, umesimama kwenye njia yangu na umenizibia njia yangu kuendelea mbele.” Basi mlima ukauliza, “Unakwenda wapi?” Swali ambalo kijito kililijibu, “Ninatafuta makazi yangu.” Mlima ukasema, “Sawa, endelea na tiririkia juu yangu!” Lakini kwa sababu kijito kilikuwa dhaifu sana na kichanga sana, hakukuwa na namna kwake kutiririka juu ya mlima mkubwa hivyo, hivyo hakikuwa na uchaguzi bali kuendelea kutiririka chini ya mlima ...

Upepo mkali ukavuma, ukiwa umekusanya mchanga na unga wa kusagika kwa mchanga kuelekea ambapo mlima ulikuwa umesimama. Upepo ukaungurumia mlima, “Hebu nipite!” Mlima ukauliza, “Unakwenda wapi?” Upepo ukavuma kwa kujibu, “Ninataka kwenda upande ule wa mlima.” Mlima ukasema, “Sawa, kama unaweza kupenya katikati yangu, basi unaweza kwenda!” Upepo mkali ukavuma huku na kule, lakini haijalishi ulikuwa mkali kiasi gani, haukuweza kupenya katikati ya mlima. Upepo ukachoka na ukaacha ili upumzike. Hivyo katika upande ule wa mlima ni upepo dhaifu tu ndio ulivuma kwa vipindi, ambao uliwafurahisha watu waliopo kule. Hiyo ilikuwa ni salamu ambayo mlima ulikuwa unaitoa kwa watu ...

Ufukweni mwa bahari, mawimbi tulivu ya bahari yalizunguka taratibu kwenye mwamba. Ghafula, wimbi kubwa likaja na likanguruma kuelekea kwenye mlima. “Pisha!” wimbi kubwa lilipiga kelele. Mlima ukauliza, “Unakwenda wapi?” Wimbi kubwa halikusita, na likaendelea kutapakaa huku likijibu, “Ninapanua eneo langu na ninataka kunyoosha mikono yangu kidogo.” Mlima ukasema, “Sawa, kama utaweza kupita juu ya kilele changu, nitakupisha njia.” Wimbi kubwa likarudi nyuma kidogo, na kisha likavurumiza kuelekea mlimani. Lakini haijalishi lilijaribu kwa nguvu kiasi gani, halikuweza kufika juu ya mlima. Halikuwa na jinsi bali kurudi nyuma taratibu kurudi kule lilipotoka ...

Kwa karne nyingi kijito kidogo kilichururika taratibu kuzunguka chini ya mlima. Kwa kufuata njia ambayo mlima uliifanya, kijito kidogo kilifanikiwa kufika nyumbani; kilijiunga na mto, na kutiririka kwenda baharini. Chini ya uangalizi wa mlima, kijito kidogo hakikuweza

kupotea. Kijito na mlima ilihimiliana na kutegemeana; ilitiana nguvu, kutenda kwa kusaidiana, na kuwepo kwa pamoja.

Kwa karne nyingi, upepo mkali haukuacha tabia yake ya kuvuma kwenye mlima. Upepo mkali ulivumisha kimbunga “ulipoutembelea” mlima kama ulivyofanya kabla. Uliutisha mlima, lakini haukuwahi kupenya katikati ya mlima. Upepo na mlima vilihimiliana na vilitegemeana; vilitiana nguvu, vilitenda kwa kusaidiana, na kuwepo kwa pamoja.

Kwa karne nyingi, wimbi kubwa wala halikupumzika, na kamwe halikuacha kupanuka. Lingenguruma na kuvurumiza tena na tena kwenda kwenye mlima, lakini mlima haukuwahi kusogea hata inchi moja. Mlima uliilinda bahari, na kwa namna hii viumbe ndani ya bahari viliongezeka na kustawi. Wimbi na mlima mkubwa vilihimiliana na vilitegemeana; vilitiana nguvu, vilitenda kwa kusaidiana, na kuwepo kwa pamoja.

Hadithi hii imeishia hapo. Kwanza, mnaweza kuniambia nini kuhusu hadithi hii, maudhui makuu yalikuwa ni nini? Kwanza kulikuwa na mlima, kijito kidogo, upepo mkali, na wimbi kubwa. Nini kilikitokea kijito kidogo na mlima mkubwa katika sehemu ya kwanza? Kwa nini tuzungumze juu ya mlima mkubwa na kijito kidogo? (Kwa sababu mlima ulikilinda kijito, kijito hakikuweza kupotea. Walitegemeana.) Unaweza kusema kuwa mlima ulikilinda au kukizuia kijito kidogo? (Ulikilinda.) Inawezekana kuwa ulikizuia? Mlima na kijito kidogo vilikuwa pamoja; ulikilinda kijito, na pia ulikuwa ni kizuizi. Mlima ulikilinda kijito ili kiweze kutiririka kwenda mtoni, lakini pia ulikizuia kutiririka kutapakaa kila sehemu ambapo kingeweza kufurika na kuwa majanga kwa watu. Hii ndiyo hoja kuu ya sehemu hii? Ulinzi wa mlima kwa kijito na kufanya kwake kazi kama kizuizi kulilinda makazi ya watu. Kisha unapata kijito kidogo kikiunganika na mto chini ya mlima na baadaye kutiririka kwenda baharini; je, huo si umuhimu wa kijito kidogo? Kijito kilipotiririka kwenda kwenye mto halafu kwenda baharini, kilikuwa kinategemea nini? Hakikuwa kinategemea mlima? Kilikuwa kinategemea ulinzi wa mlima na mlima kufanya kazi kama kizuizi; je, hii ndiyo hoja kuu? Je, mnauona umuhimu wa milima kwa maji katika tukio hili? Je, Mungu ana makusudi Yake ya kutengeneza milima mirefu na mifupi? (Ndiyo.) Hii ni sehemu ndogo ya hadithi, na kutoka tu katika kijito kidogo na mlima mkubwa tunaweza kuona thamani na umuhimu wa Mungu kuviumba vitu hivi viwili. Tunaweza pia kuona hekima Yake na makusudi katika jinsi ya kutawala vitu hivi viwili. Sivyo?

Sehemu ya pili ya hadithi inashughulika na nini? (Upepo mkali na mlima mkubwa.) Je, upepo ni kitu kizuri? (Ndiyo.) Sio lazima, kwa kuwa wakati mwingine ikiwa upepo ni mkali sana unaweza kuwa janga. Ungejisikiaje kama ungelazimika kukaa nje kwenye upepo mkali? Inategemea na ukali wake, sivyo? Kama ulikuwa upepo wa kiwango cha tatu au cha nne ungeweza kuvumilika. Kwa kiasi cha juu zaidi, mtu angeweza kupata shida kuendelea kuacha

macho wazi bila kufumba. Lakini ungeweza kuvumilia kama upepo ungevuma kwa nguvu na kuwa kimbunga? Usingeweza kuvumilia. Hivyo, ni kosa watu kusema kwamba siku zote upepo ni mzuri, au kwamba siku zote ni mbaya kwa sababu inategemeana na upepo ni mkali kiasi gani. Hivyo mlima una matumizi gani hapa? Je, kwa kiasi fulani haufanyi kazi kama kichujio cha upepo? Mlima unachukua upepo mkali na kuutuliza na kuwa nini? (Upepo mwanana.) Watu wengi wanaweza kuugusa na kuuhisi katika mazingira ambamo wanaishi—je, wanachohisi ni upepo mkali au upepo mwanana? (Upepo mwanana.) Je, hili sio kusudi mojawapo la Mungu la kuumba milima? Ingekuwaje ikiwa watu wangeishi katika mazingira ambapo mchanga ulipeperuka sana katika upepo, bila kuzuiliwa na bila kuchujwa? Je, inaweza kuwa kwamba ardhi inayokabiliwa na mchanga na mawe yanayopeperuka haingeweza kukalika? Mawe yanaweza kuwapiga watu, na mchanga unaweza kuwapofusha. Upepo unaweza kuwaangusha watu au kuwabeba hewani. Je, upepo mkali una thamani? Niliposema kuwa ni mbaya, basi watu wangepeweza kuhisi kwamba hauna thamani, lakini hiyo ni sahihi? Je, kubadilika kuwa upepo mwanana hakuna thamani? Watu wanahitaji nini zaidi kunapokuwa na unyevunyevu au kusongwa? Wanahitaji upepo mwanana kuwapepea, kuchangamsha na kusafisha vichwa vyao, kuamsha kufikiria kwao, kurekebisha na kuboresha hali zao za akili. Kwa mfano, nyote mmekaa chumbani kukiwa na watu wengi na hewa sio safi, ni kitu gani mtakihitaji zaidi? (Upepo mwanana.) Katika maeneo ambapo hewa imetibuliwa na imejaa uchafu inaweza kushusha uwezo wa kufikiri wa mtu, kupunguza mzunguko wao wa damu, na kuwafanya vichwa vyao visiwe vyepesi. Hata hivyo, hewa itakuwa safi ikiwa itapata nafasi ya kujongea na kuzunguka na watu watajihisi nafuu zaidi. Ingawa kijito kidogo na upepo mkali vingeweza kuwa janga, alimradi mlima upo utavibadilisha na kuwa vitu ambavyo kwa kweli vinawanufaisha watu; hiyo si kweli?

Sehemu ya tatu ya hadithi inazungumzia nini? (Mlima mkubwa na wimbi kubwa.) Mlima mkubwa na wimbi kubwa. Mandhari hapa ni mlima mkubwa uliopo kando ya bahari ambapo tunauona mlima, mawimbi tulivu ya bahari, na pia wimbi kubwa. Mlima ni nini kwa wimbi hapa? (Mlinzi na kinga.) Ni mlinzi na pia ni kinga. Lengo la kulinda ni kuilinda sehemu hii ya bahari isipotee ili kwamba viumbe vinavyoishi ndani yake viweze kuishi, kuongezeka na kustawi. Kama kinga, mlima hulinda maji ya bahari—chanzo hiki cha maji—yasifurike na kusababisha janga, ambalo linaweza kudhuru na kuharibu makazi ya watu. Hivyo tunaweza kusema kwamba mlima ni kinga na mlinzi. Hii inaonyesha hali ya kutegemeana kati ya mlima na kijito, mlima na upepo mkali, na mlima na wimbi kubwa, na jinsi vinavyozuiliana na kutegemeana, ambayo nimezungumzia.

Huu ni umuhimu wa muungano kati ya mlima mkuu na kijito kidogo, mlima mkuu na upepo mkali, na mlima mkuu na wimbi kubwa kabisa; huu ndio umuhimu wa kutiana nguvu na kuhimiliana, na kuwepo kwao pamoja. Vitu hivi ambavyo nimezungumzia. Kuna kanuni na

sheria inayoongoza vitu hivi ambavyo Mungu aliviumba kuendelea kuishi. Mnaweza kuona kile ambacho Mungu alifanya kutokana na kile kilichotokea kwenye hadithi? Je, Mungu aliumba ulimwengu na kupuuzia kile kilichotokea baada ya hapo? Je, Alitoa kanuni na kuunda namna ambazo wao hufanya kazi na halafu kuwapuuza baada ya hapo? Je, hicho ndicho kilichotokea? (Hapana.) Ni nini hicho sasa? Mungu bado Anadhibiti maji, upepo na mawimbi. Haviachi bila kudhibitiwa, wala haviachi visababishe madhara au kuharibu nyumba ambamo watu wanaishi. Kwa sababu ya hili, watu wanaweza kuendelea kuishi na kuongezeka na kusitawi katika nchi. Kitu kinachomaanisha kwamba Mungu alikwishapanga kanuni kwa ajili ya kuishi Alipofanya mbingu. Mungu Alipotengeneza vitu hivi, Alihakikisha kwamba vingewanufaisha binadamu, na pia Alividhibiti ili kwamba visiwe shida au majanga kwa binadamu. Ikiwa havingesimamiwa na Mungu, je, maji yangetiririka kila mahali? Je, upepo usingevuma kila sehemu? Yanafuata sheria? Ikiwa Mungu hakuvisimamia visingeongozwa na kanuni yoyote, na upepo ungevuma na maji yangeinuka na kutiririka kila sehemu. Ikiwa wimbi kubwa lingekuwa refu kuliko mlima, je, sehemu hiyo ya bahari ingekuwa bado ipo? Bahari isingeweza kuwepo. Ikiwa mlima haungekuwa mrefu kama wimbi, eneo la bahari lisingekuwepo na mlima ungepoteza thamani na umuhimu wake.

Je, unaiona hekima ya Mungu katika visa viwili hivi? Mungu aliumba ulimwengu na ni Bwana wake; Anaisimamia yote na Yeye huruzuku vyote, na ndani ya vitu vyote, Yeye huona na kuchunguza kila neno na tendo la kila kitu kilichopo. Vivyo hivyo, pia, ndivyo Mungu huona na kuchunguza kila kona ya maisha ya wanadamu. Hivyo, Mungu anajua kwa undani kila kipengele cha kila kitu kilichopo ndani ya uumbaji Wake, kutoka kwa kazi ya kila kitu, asili yake, na sheria zake za kuishi hadi kwa umuhimu wa maisha yake na thamani ya kuwepo kwake, yote haya Mungu anayajua kwa ukamilifu. Mungu Aliuumba ulimwengu; unadhani Anapaswa kufanya utafiti juu ya kanuni hizi zinazouongoza ulimwengu? Je, Mungu Anahitajika kusoma maarifa au sayansi ya kibinadamu kufanya utafiti na kuyaelewa? (Hapana.) Je, kuna yeyote miongoni mwa binadamu aliye na elimu na maarifa ya kuelewa mambo yote kama Mungu Anavyoelewa? Hakuna, sivyo? Je, kuna mamajusi au wanabiolojia ambao wanaelewa kweli sheria ambazo kwazo vitu vinaishi na kukua? Je, wanaweza kweli kuelewa thamani ya uwepo wa kila kitu? (Hawawezi.) Hii ni kwa sababu vitu vyote viliumbwa na Mungu, na haijalishi ni kwa kiasi kikubwa au kwa kina kiasi gani binadamu anajifunza maarifa haya, au ni kwa muda mrefu kiasi gani wanajitahidi kujifunza, hawataweza kuelewa siri na makusudi ya uumbaji wa Mungu wa vitu vyote, hiyo si sahihi? Baada ya kujadili kwa kina hadi sasa, mnahisi kwamba mna ufahamu wa juujuu wa maana ya kweli ya kirai: “Mungu ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote”? (Ndiyo.) Nilijua kwamba Nilipojadili mada hii watu wengi wangefikiri kwa haraka juu ya “Mungu ni ukweli, na Mungu hutumia neno Lake kutukimu,” lakini wangeifikiria tu katika kiwango hiki.

Baadhi hata wangehisi kwamba Mungu kukimu maisha ya binadamu, kutoa chakula na kinywaji cha kila siku na mahitaji yote ya kila siku haihesabiki kama Yeye kumkimu mwanadamu. Je, baadhi ya watu hawahisi namna hii? Lakini, je, si nia ya Mungu katika uumbaji Wake ni wazi kabisa—kuwaruhusu binadamu wawepo na kuishi kwa kawaida? Mungu anadumisha mazingira ambamo watu wanaishi na anatoa vitu vyote ambavyo binadamu anahitaji ili kuishi. Aidha, Anasimamia na kuwa mkuu juu ya vitu vyote. Haya yote yanamfanya binadamu kuishi na kusitawi na kuongezeka kwa kawaida; ni kwa njia hii ndipo Mungu Anavikimu vitu vyote na binadamu. Je, watu hahitaji kutambua na kuelewa mambo haya? Pengine baadhi wanaweza kusema, “Mada hii ipo mbali sana na maarifa yetu juu ya Mungu Mwenyewe wa kweli, na hatutaki kujua hili kwa sababu binadamu hawezi kuishi kwa mkate pekee, lakini badala yake anaishi kwa neno la Mungu.” Hili ni sahihi? (Hapana.) Kosa ni lipi hapa? Je, mnaweza kuwa na uelewa kamili juu ya Mungu ikiwa mnaelewa tu vitu ambavyo Mungu amesema? Ikiwa mnakubali tu kazi Yake na hukumu Yake na kuadibu, je, mtakuwa na uelewa kamili juu ya Mungu? Ikiwa mnaelewa sehemu ndogo tu ya tabia ya Mungu, sehemu ndogo ya mamlaka ya Mungu, hiyo inatosha kupata uelewa juu ya Mungu, sio? (Hapana.) Matendo ya Mungu yanaanza na uumbaji Wake wa ulimwengu na yanaendelea leo ambapo matendo yake ni dhahiri muda wote na kila wakati. Ikiwa watu wanaamini kwamba Mungu yupo kwa sababu tu Amewachagua baadhi ya watu ambao kwao Anafanya kazi Yake kuwaokoa watu hao, na kwamba hakuna kingine chochote kinachohusiana na Mungu, si mamlaka Yake, hadhi Yake, wala matendo Yake, basi, je, mtu anaweza kuchukuliwa kuwa aliye na ufahamu wa kweli kwa Mungu? Watu walio na haya yanayodaiwa kuwa “maarifa ya Mungu” wana ufahamu wa upande mmoja tu, ambao wanatumia kuzuia matendo Yake kwa kundi moja la watu. Je, haya ni maarifa ya kweli juu ya Mungu? Sio kwamba watu wenye aina hii ya maarifa juu ya Mungu wanakataa uumbaji Wake wa vitu vyote na utawala wao juu Yao? Baadhi ya watu hawatamani kujishughulisha na hili jambo, wakijiwazia badala yake: “Sioni utawala wa Mungu juu ya vitu vyote, ni kitu ambacho kipo mbali sana na mimi na sitaki kukielewa. Mungu Anafanya kile anachotaka na wala hakinihusu. Ninakubali tu uongozi wa Mungu na neno Lake ili niweze kuokolewa na kufanywa mkamilifu na Mungu. Hakuna kingine kilicho na umuhimu kwangu. Sheria ambazo Mungu Alifanya Alipoviumba vitu vyote na kile ambacho Mungu Anafanya kuvikimu vitu vyote na kumkimu mwanadamu havinihusu.” Haya ni mazungumzo ya aina gani? Je, huu si uasi? Hii sio fedheha kabisa? Je, kuna mtu yeyote miongoni mwenu aliye na ufahamu kama huu? Ninajua kwamba kuna watu wengi sana wanaofikiri namna hii hata kama hamtasema. Aina ya mtu huyu wa kuamini katika maandiko anaweza kutumia kile kinachoitwa msimamo wao wa kiroho katika namna wanavyotazama kila kitu. Wanataka kumwekea Mungu mipaka katika Biblia, kumwekea Mungu mipaka kwa maneno Aliyoyazungumza, na kumwekea Mungu mipaka katika neno lilikoandikwa. Hawatamani kufahamu zaidi kuhusu Mungu na hawataki

Mungu Aweke umakini zaidi katika kufanya mambo mengine. Aina hii ya kufikiri ni ya kitoto na ni ya kidini sana. Je, watu wenye mitazamo hii wanaweza kumjua Mungu? Wanaweza kuwa na wakati mgumu kumjua Mungu. Leo nimesimulia hadithi mbili, kila moja ikigusia kipengele tofauti. Mnaweza kuhisi kwamba ni za kina au hata ni za kidhahania kidogo na ngumu kutambua na kufahamu. Inaweza kuwa ni vigumu kuzihusianisha na matendo ya Mungu na Mungu Mwenyewe. Hata hivyo, matendo yote ya Mungu na yote Aliyoyafanya miongoni mwa vitu vyote na miongoni mwa binadamu wote yanapaswa kueleweka kwa wazi na kwa usahihi kwa kila mtu na kwa kila mmoja ambaye anatafuta kumjua Mungu. Maarifa haya yatakupatia uthibitisho wa imani katika uwepo wa kweli wa Mungu. Pia yatakupatia maarifa sahihi juu ya hekima ya Mungu, nguvu Zake, na jinsi ambavyo anakimu vitu vyote. Itakufanya uelewe kwa wazi kabisa uwepo wa kweli wa Mungu na kuona kwamba siyo hadithi ya kubuni, na sio kisasili. Hii inakufanya uone kwamba si ya kidhahania, na sio tu nadharia, na kwamba Mungu hakika sio tu riziki ya kiroho, lakini ni kweli yupo. Aidha, itawaruhusu watu kujua kwamba Mungu daima amekimu viumbe na binadamu wote; Anafanya hivi kwa njia Yake mwenyewe na kulingana na wizani Wake mwenyewe. Hivyo mtu anaweza kusema kwamba ni kwa sababu Mungu Aliumba vitu vyote na Akavipatia kanuni kwamba kwa amri Yake kila kimoja kinafanya kazi zake kilizopangiwa, vinatimiza majukumu yao, na kutimiza jukumu ambalo lilipewa kila kimoja. Vitu vyote vinatimiza jukumu lao kwa ajili ya binadamu, na hufanya hivi katika sehemu, mazingira ambamo watu wanaishi. Ikiwa Mungu hangefanya mambo namna hii na mazingira ya binadamu hayangekuwa jinsi yalivyo, imani ya watu kwa Mungu au wao kumfuata Yeye—hakuna ambacho kingewezekana; yangekuwa tu mazungumzo ya bure, hii sio sahihi?

Hebu tuchukue mtazamo mwingine katika hadithi hii ambayo tumekwishaisikia—mlima mkubwa na kijito kidogo. Mlima una matumizi gani? Viumbe hai vinastawi juu ya mlima hivyo kuna thamani ya uwepo wake kwa wenyewe. Wakati huo huo, mlima unazuia kijito kidogo, unahakikisha kuwa hakitiririki kuelekea mahali popote kinapotaka na hivyo kuleta janga kwa watu. Hii sio sahihi? Uwepo tu wa mlima unaruhusu viumbe hai kama vile miti na majani na mimea yote mingine na wanyama mlimani kustawi huku pia ukiongoza kijito kidogo kinapopaswa kutiririka; mlima unakusanya maji ya kijito na kuyaongoza kiasili kuzunguka chini yake ambapo yanaweza kutiririka kuelekea mtoni na hatimaye baharini. Kanuni zilizopo hapa hazikutengenezwa na asili, badala yake zilipangwa mahususi na Mungu wakati wa uumbaji. Kuhusu mlima mkubwa na upepo mkali, mlima pia unahitaji upepo. Mlima unahitaji upepo ili kupapasa viumbe hai ambao wanaishi juu yake, na wakati huo huo mlima unazuia jinsi ambavyo upepo unaweza kuvuma kwa nguvu ili kwamba usiharibu na kuteketeza. Kanuni hii inashikilia wajibu wa mlima mkubwa, hivyo kanuni hii kuhusiana na wajibu wa mlima ilipata umbo yenyewe? (Hapana.) Badala yake ilitengenezwa na Mungu. Mlima mkubwa una wajibu wake na

upepo mkali una wajibu wake pia. Sasa, kuhusu mlima mkubwa na wimbi kubwa, je, bila mlima kuwa pale maji yangepata mwelekeo wake wa kutiririka yenyewe? (Hapana.) Maji pia yangefurika. Mlima una thamani yake ya kuwepo kama mlima, na bahari ina thamani yake ya kuwepo kama bahari; hata hivyo, chini ya mazingira haya ambapo yanaweza kuwepo pamoja kwa kawaida na ambapo kila kimoja hakiingiliani na kingine, pia vinadhibitiana; mlima mkubwa unadhibiti bahari ili isiweze kufurika na hivyo unalinda makazi ya watu, na hii pia inaruhusu bahari kulea viumbe hai vinavyokaa ndani yake. Je, hii sura ya nchi ilipata umbo yenyewe? (Hapana.) Pia iliumbwa na Mungu. Tunaona katika taswira hizi kwamba Mungu Alipoiumba dunia, Alijua kabla mahali ambapo mlima ungesimama, mahali ambapo kijito kingetiririka, kutoka katika mwelekeo ambapo upepo mkali ungeanza kuvuma na kuelekea ambapo ungekwenda, vile vile kiwango cha urefu ambao wimbi lingekuwa. Nia na makusudi ya Mungu yamekumbatiwa ndani ya vitu vyote hivi na ni matendo Yake. Sasa, unaweza kuona kwamba matendo ya Mungu yapo katika vitu vyote? (Ndiyo.)

Kusudi la mjadala wetu wa haya mambo ni nini? Je, ni ili kwamba watu waweze kutafiti kanuni zilizopo kwenye uumbaji wa Mungu wa ulimwengu? Je, ni ili kwamba watu wavutiwe na falaki na jiografia? (Hapana.) Sasa ni nini? Ni ili kwamba watu wataelewa matendo ya Mungu. Katika matendo ya Mungu, watu wanaweza kukubali na kuthibitisha kwamba Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote. Kama unaweza kuielewa hoja hii, basi utaweza kuthibitisha kweli nafasi ya moyoni mwako na utaweza kuthibitisha kwamba Mungu ni Mungu Mwenyewe wa kipekee, Muumbaji wa mbingu na nchi na vitu vyote. Hivyo, je, inasaidia katika uelewa wako juu ya Mungu kujua kanuni za vitu vyote na kujua matendo ya Mungu? (Ndiyo.) Inasaidiaje? Kwanza, utakapojua matendo haya ya Mungu, bado utavutiwa na falaki na jiografia? Bado utakuwa na moyo wa kushuku na mashaka kwamba Mungu ni Muumbaji wa vitu vyote? Bado utakuwa na moyo wa mtafiti na mashaka kwamba Mungu ni Muumbaji wa vitu vyote? (Hapana.) Utakapothibitisha kwamba Mungu ni Muumbaji wa ulimwengu na zaidi ujue kanuni zilizopo katika uumbaji Wake, moyoni mwako kweli utaamini kwamba Mungu anakimu ulimwengu? (Ndiyo.) Je, “kukimu” hapa lina maana mahsusi, au linarejelea hali mahsusi? Kwamba Mungu anakimu ulimwengu ina maana na matumizi mapana sana. Mungu hawakimu tu watu kwa kuwapatia mahitaji yao ya kila siku ya chakula na kinywaji, Anawapatia wanadamu kila kitu wanachohitaji, ikiwa ni pamoja na kila kitu ambacho watu wanakiona na vitu ambavyo haviwezi kuonekana. Mungu anatetea, anasimamia na anatawala mazingira ya kuishi ambayo binadamu anahitaji. Mazingira yoyote ambayo binadamu anayataka katika msimu wowote, Mungu ameyaandaa. Angahewa au halijoto yoyote ambayo inafaa kwa ajili ya uwepo wa binadamu pia ipo chini ya uadhibiti wa Mungu na hakuna kati ya kanuni hizi ambayo inatokea yenyewe tu au bila utaratibu; ni matokeo ya kanuni ya Mungu na matendo Yake. Mungu Mwenyewe ni chanzo

cha kanuni zote hizi na ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote. Huu ni ukweli uliothibitishwa na usioweza kushambuliwa na haijalishi unauamini au huuamini, haijalishi unaweza kuuona au huwezi kuuona, au haijalishi unaweza kuuelewa au huwezi kuuelewa.

Ninajua kwamba watu wengi wanaamini tu maneno na kazi ya Mungu ambayo yako katika Biblia. Kwa watu wachache, Mungu amefichua matendo Yake na akawawezesha watu waone thamani ya uwepo Wake. Pia anawawezesha wawe na ufahamu kiasi wa utambulisho Wake na Akathibitisha ukweli wa uwepo Wake. Hata hivyo, kwa watu wengi zaidi, ukweli kwamba Mungu Aliuumba ulimwengu na kwamba Anasimamia na kukimu vitu vyote unaonekana kuwa usio dhahiri au wenye utata na hata wanakuwa na mtazamo wa mashaka. Aina hii ya mtazamo inawafanya watu kuendelea kuamini kwamba sheria za ulimwengu asilia zilijitengeneza zenyewe, kwamba mabadiliko, mageuzi na ajabu ya ulimwengu asilia na sheria ambazo zinaongoza asili ziliibuka kwa hiari yao. Maana yake hii ni kwamba katika akili za watu, hawawezi kufikiri jinsi ambavyo Mungu alitengeneza kanuni juu ya vitu vyote, hawawezi kuelewa jinsi ambavyo Mungu anasimamia na kuvihudumia vitu vyote. Kwa sababu ya mipaka ya kigezo hiki, watu hawawezi kuamini kwamba Mungu aliumba, anatawala, na hukimu vitu vyote; hata wale wanaoamini wamewekewa mipaka katika imani yao katika Enzi ya Sheria, Enzi ya Neema na Enzi ya Ufalme; wanaamini kwamba matendo ya Mungu na ruzuku Yake kwa binadamu ni kwa ajili tu ya wateule Wake. Hiki ni kitu ambacho Nachukia kukiona na kinaleta maumivu makali sana, kwa sababu binadamu hufurahia yote ambayo Mungu huleta, halafu wakati huohuo wanakana yote ambayo Anafanya na yote ambayo Anawapatia. Watu wanaamini tu kwamba mbingu na nchi na vitu vyote vinaongozwa na kanuni zao za asili na kwa sheria zao za asili na kwamba hazina mtawala wa kuvidhibiti au mtawala yeyote wa kuzikimu na kuzilinda. Hata kama unamwamini Mungu, unaweza usiamini yote haya kuwa ni maneno Yake; hili ni eneo kati ya maeneo ambayo hayajapewa uzito kwa kila anayemwamini Mungu, kwa kila mtu ambaye anakubali neno la Mungu, na kila mtu anayemfuata Mungu. Hivyo, Ninapoanza tu kujadili kitu fulani ambacho hakihusiani na Biblia au kile kinachodaiwa kuwa istilahi ya kiroho, baadhi ya watu wanasumbuliwa au wanachoshwa au hata kutofurahia. Wanahisi kwamba maneno Yangu yanaonekana yaliyotengana na watu wa kiroho na mambo ya kiroho. Hicho ni kitu kibaya. Linapokuja suala la kujua matendo ya Mungu, hata kama hatutaji falaki, jiografia, au biolojia, tunajua utawala wa Mungu juu ya vitu vyote, tunajua kukimu Kwake vitu vyote, na kwamba Yeye ni chanzo cha vitu vyote. Hii ni kazi muhimu sana na ambayo inapaswa kuchunguzwa, mmelewa?

Kuhusu hadithi mbili ambazo Nimezisema, ingawa zinaweza kuwa na maudhui ambayo si ya kawaida na zinaweza kuwa zimesimuliwa na kuwasilishwa kwako kwa mtindo wa kipekee, hata hivyo Nilitaka kutumia lugha ya moja kwa moja na njia rahisi ili kwamba ungeweza

kukubali na kuelewa kitu ambacho ni cha kina zaidi. Hili ndilo lilikuwa lengo langu tu. Nilitaka mwone na kuamini kuwa Mungu ni Mtawala wa vitu vyote kutokana na hadithi hizi ndogo na matukio. Lengo la kusimulia hadithi hizi ni kuwafanya mwone na kujua matendo ya Mungu yasiyokuwa na kikomo ndani ya hadithi yenye kikomo. Kuhusu ni lini mtafikia kikamilifu matokeo haya ndani yenu inategemea uzoefu wako binafsi na maendeleo yako binafsi. Ukifuatilia ukweli na ikiwa unatafuta kumjua Mungu, basi mambo haya yatafanya kazi kama kumbusho lenye nguvu na imara kwako; yatakufanya uwe na utambuzi wa kina sana, ubayana katika uelewa wako, na polepole utasogea karibu na matendo ya kweli ya Mungu, ukaribu ambao utakuwepo bila umbali na bila hitilafu. Hata hivyo, kama hutafuti kumjua Mungu, basi hadithi hizo ulizozisikia haziwezi kukudhuru. Mnaweza kuzichukulia kama hadithi za kweli.

Je, mlielewa kitu chochote kwenye hadithi hizi mbili? Kwanza, je, hadithi hizi mbili zinajitenga na mjadala wetu wa awali kuhusu Mungu kumjali binadamu? Je, kuna uhusiano usioepukika? Je, ni kweli kwamba ndani ya hadithi hizi mbili tunaona matendo ya Mungu na kujali kwa kiwango kikubwa Anakokipa kila kitu Anachopanga kwa ajili ya binadamu? Je, ni kwamba kila kitu ambacho Mungu Anafanya na mawazo Yake yote yanaelekezwa kwa uwepo wa binadamu? (Ndiyo.) Je, sio kwamba fikra makini za Mungu na kujali kwake binadamu kuko dhahiri? Binadamu hana haja ya kufanya chochote. Mungu amewaandaliwa watu hewa—kile wanachohitaji kufanya ni kuivuta tu. Mboga na matunda wanayokula vinapatikana kwa urahisi. Kutoka kaskazini hadi kusini, kutoka mashariki hadi magharibi, kila kanda ina rasilimali zake asili na mazao na matunda tofauti na mboga zimeandaliwa na Mungu. Tukizungumza juu ya mazingira mapana, Mungu aliumba vitu vyote viimarishane, vitegemeane, vitiane nguvu, vishindane na viishi pamoja. Hii ni mbinu Yake na sheria Yake ya kudumisha kuendelea kuishi na kuwepo kwa vitu vyote; kwa njia hii, binadamu ameishi kwa utulivu na kwa amani na amekua na kuzaliana kutoka kizazi kimoja hadi kingine katika mazingira haya hai hadi siku ya leo. Yaani, Mungu anaweka uwiano katika mazingira ya asili. Kama kusingekuwa na udhibiti na ukuu wa Mungu, hakuna mwanadamu ambaye angeweza kudumisha na kuweka wiano katika mazingira, hata kama bado yangukuwa yaliumbwa na Mungu, bado yangukuwa zaidi ya uwezo wa mtu yeyote kuyalinda na kuyaweka katika usawa. Katika baadhi ya maeneo hakuna hewa, hivyo watu hawawezi kuishi hapo na Mungu hatakuruhusu uende kwa wao. Hivyo, usivuke mipaka inayostahili. Hili ni kwa ajili ya usalama wa binadamu—kuna siri ndani yake. Kila kipengele cha mazingira, urefu na upana wa dunia, na kila kiumbe hai duniani—vilivyo hai na vilivyokufa—viliandaliwa na Mungu na Alivifikiria: Kwa nini kitu hiki kinahitajika? Kwa nini sio cha lazima? Lengo la kuwa na kitu hiki hapa ni nini na kwa nini kiende hapo? Mungu alikuwa amekwishafikiria hii yote na hakuna haja ya watu kuyafikiria. Kuna baadhi ya watu wapumbavu ambao siku zote wanafikiri juu ya kuhamisha milima, lakini badala ya kufanya

hivyo, kwa nini wasihamie kwenye tambarare? Kama huipendi milima, kwa nini unakwenda kuishi karibu nayo? Huu si upumbavu? Nini hutokea ikiwa utauhamisha mlima huo? Kimbunga kikali kitavuma au wimbi kubwa litapiga na makazi ya watu yataharibiwa. Je, hicho kisingekuwa kitu cha kipumbavu kufanya? Watu wanaweza tu kuharibu. Hawawezi hata kudumisha pahali pa pekee waliponapo pa kuishi, na ilhali wanataka kukimu vitu vyote. Hili haliwezekani.

Mungu anamwacha mwanadamu kusimamia vitu vyote na kuwa na utawala juu yao, lakini mwanadamu anafanya kazi nzuri? Mwanadamu ana tabia ya uharibifu; mwanadamu sio kwamba tu hawezi kutunza vitu kama Mungu alivyoviumba, kwa kweli ameviharibu. Binadamu ameifanya milima kuwa vifusi, ameijaza bahari kwa mchanga, na amezibadilisha tambarare kuwa majangwa ambapo hakuna kinachoweza kuishi. Halafu katika majangwa hayo mwanadamu amejenga viwanda na kujenga vinu vya nyuklia na uharibifu unaendelea katika pande zote. Mito si mito tena, bahari si bahari tena.... Binadamu anapovunja uwiano na kanuni za maumbile, siku yao ya maafa na kifo haipo mbali na haiepukiki. Maafa yanapokuja, watajua viumbe vya Mungu ni vya thamani kiasi gani jinsi vyote ni muhimu kwa binadamu. Mwanadamu kuishi katika mazingira yenye hali ya hewa nzuri ni sawa na kuwa peponi. Watu hawatambui baraka hii, lakini wakati ambapo wataipoteza yote ndipo watatambua ni jinsi gani yote ni adimu na ya thamani. Ni kwa jinsi gani mtu anaweza kuirudisha hii yote? Watu wangepanyaje ikiwa Mungu Asingekuwa tayari kuitengeneza tena? Mnggefanyaje? (Tusingeweza kufanya chochote.) Kwa kweli, kuna kitu mnachoweza kufanya na ni rahisi sana na Nitakapowaambia ni nini, mara moja mtajua kwamba hiyo inawezekana. Kwa nini mwanadamu amejikuta katika mashaka yake ya kimazingira ya sasa? Je, ni kwa sababu ya tamaa na uharibifu wa mwanadamu? Ikiwa mwanadamu atasitisha uharibifu huu, je, mazingira ya kuishi hayatakuwa sawa taratibu yenyewe? Ikiwa Mungu hafanyi chochote, ikiwa Mungu hatamani tena kufanya kitu chochote kwa ajili ya binadamu—yaani, hataki kuingilia—njia bora zaidi ingekuwa ni binadamu kusitisha uharibifu huu na kurudisha vitu kuwa vile vilivyokuwa. Kusitisha uharibifu huu wote humaanisha kusitisha uporaji na uharibifu wa vitu ambavyo Mungu ameviumba. Hii itaruhusu mazingira ambamo mwanadamu anaishi kuboreka taratibu. Kushindwa kufanya hivyo kutasababisha uharibifu zaidi wa mazingira na hali itakuwa mbaya zaidi. Je, mbinu Yangu ni rahisi? Ni rahisi na inawezekana, siyo? Ni rahisi kweli, na inawezekana kwa baadhi ya watu, lakini je, hii inawezekana kwa watu walio wengi duniani? (Haiwezekani.) Kwenu nyinyi, angalau inawezekana? (Ndiyo.) Chanzo cha “ndiyo” yenu ni nini? Je, mtu anaweza kusema kuwa inahusisha kuanzisha msingi wa uelewa kuhusu matendo ya Mungu? Je, mtu anaweza kusema inahusisha kushikilia kanuni na mpango wa Mungu? (Ndiyo.) Kuna njia ya kubadilisha haya yote, lakini hiyo siyo mada tunayoijadili sasa. Mungu anawajibika kwa kila uhai wa binadamu na anawajibika hadi mwisho. Mungu Anawakimu, hata kama

umeugua kutokana na mazingira yaliyoharibiwa na Shetani, au kuathiriwa na uchafuzi au kupata madhara mengine, haijalishi; Mungu Anakukimu na Atakuacha uendelee kuishi. Je, una imani katika hili? (Ndiyo.) Mungu hachukulii upotevu wa maisha ya binadamu kwa urahisi.

Mmehisi umuhimu wa kumtambua Mungu kama chanzo cha uhai kwa vitu vyote? (Ndiyo, tumehisi.) Mna hisia gani? Endelea, nitasikiliza. (Hapo awali, hatukufikiria kamwe kuhusisha milima, bahari na maziwa na matendo ya Mungu. Haikuwa hadi tuliposikia ushirika wa Mungu leo ndipo tulielewa kwamba vitu hivi vina matendo na hekima ya Mungu ndani yavyo; tunaona kwamba hata wakati ambapo Mungu alianza kuumba vitu vyote, Alikuwa tayari amekijaza kila kitu na hatima na nia Yake njema. Vitu vyote vinaimarishana na kutegemeana na binadamu ndiye anayenufaika mwishowe. Tulichokisikia leo kinaonekana ni kipya na kigeni, na tumehisi jinsi ambavyo matendo ya Mungu ni halisi. Katika dunia halisi, katika maisha yetu ya kila siku, na katika mwingiliano wetu na vitu vyote, tunaona kwamba hili liko hivyo) Unaiona kabisa, sio? Mungu kumkimu binadamu sio bila msingi imara, hatamki tu maneno machache na kuishia hapo tu. Mungu anafanya mambo mengi, hata vitu ambavyo huvioni anafanya kwa manufaa yako. Mwanadamu anaishi katika mazingira haya, ulimwengu huu ambao Mungu Aliutengeneza, na ndani yake watu na vitu vingine vinategemeana, kama tu ambavyo gesi inayotoka kwenye mimea inaitakasa hewa na kuwanufaisha watu wanaoivuta. Hata hivyo, baadhi ya mimea ni yenye sumu kwa watu, ilhali mimea mingine inakinza mimea yenye sumu. Haya ni maajabu ya uumbaji wa Mungu! Lakini hebu tuiache mada hii kwa sasa; leo, mjadala wetu hasa ulihusu kuishi pamoja kwa mwanadamu na viumbe vingine, ambavyo mwanadamu hawezi kuishi bila. Ni nini umuhimu wa uumbaji wa Mungu wa vitu vyote? Mwanadamu hawezi kuishi bila vitu vingine, kama ambavyo mwanadamu anahitaji hewa kuweza kuishi na namna ambavyo kama ungewekwa kwenye ombwe ungekufa upesi. Hii ni kanuni ya msingi sana kukufanya kuona kwamba mwanadamu anahitaji vitu vingine. Hivyo ni aina gani ya mtazamo ambao mwanadamu anapaswa kuwa nao kwa vitu vyote? Vithamini sana, vitunze, vitumie kwa ufanisi, usiviharibu, usivipoteze, na usivibadilishe kwa ghafula, maana vitu vyote vinatoka kwa Mungu na vinatolewa kwa binadamu na binadamu anapaswa kuvichukulia kwa uangalifu. Leo tumejadili mada hizi mbili, na mtarudi na kuzitafakari kwa kina. Wakati ujao tutajadili vitu vingi zaidi kwa kina. Ushirika wetu utaishia hapa kwa leo. Kwa heri! (Kwa heri!)

Januari 18, 2014

Tanbihi:

a. Mtu/kitu kinachodhihirisha uzuri/ubora wa kingine kwa kuvilinganisha.

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee VIII

Mungu ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote (II)

Tuendeleo na mada ya mawasiliano ya wakati uliopita. Je, mnaweza kukumbuka ni mada gani tuliwasiliana wakati uliopita? (Mungu Ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote.) Je, “Mungu Ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote” ni mada mnayohisi ikiwa mbali sana nanyi? Je, una ufahamu wowote wa juujuu kuhusu jambo hilo? Mtu fulani anaweza kuniambia wazo kuu la mada hii tuliowasiliana wakati uliopita? (Kupitia kwa uumbaji wa Mungu wa vitu vyote, ninaona kwamba Mungu hulea vitu vyote na hulea wanadamu. Katika siku zilizopita, kila mara nilifikiria kwamba Mungu anapompa mwanadamu, Anawapa tu watu Wake waliochaguliwa neno Lake, lakini kamwe sikuona, kupitia kwa sheria za vitu vyote, kwamba Mungu anawalea wanadamu. Ni kupitia tu kwa mawasiliano ya Mungu ya kipengele hiki cha ukweli ndipo nimehisi kwamba Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote na uhai wa vitu vyote unapewa na Mungu, kwamba Mungu anatengeneza sheria hizi, na kwamba Anavilea vitu vyote. Kutokana na uumbaji Wake wa vitu vyote ninaona upendo wa Mungu.) Wakati uliopita, kimsingi tuliwasiliana kuhusu uumbaji wa Mungu wa vitu vyote na jinsi Aliunda sheria na kanuni kwa ajili ya vitu hivyo. Chini ya sheria hizi na chini ya kanuni hizi, vitu vyote huishi na kufa na mwanadamu na kuishi pamoja kwa amani na mwanadamu chini ya utawala wa Mungu na machoni pa Mungu. Kwanza tulizungumza kuhusu Mungu kuumba vitu vyote na kutumia mbinu Zake kuamua sheria zao za ukuaji na vilevile njia na mpangilio wa ukuaji wao. Pia aliamua njia njia ambazo vitu vyote huendelea kuishi katika ardhi hii, ili viweze kuendelea kukua na kuzaana na kutegemeana kwa ajili ya kuendelea kuishi. Kwa mbinu na sheria hizi, vitu vyote vinaweza kuwepo na kukua katika nchi hii kwa ufanisi na kwa amani. Ni kwa kuwa tu na mazingira kama haya ndipo wanadamu wanaweza kuwa na makao na mazingira ya kuishi yaliyo thabiti, na chini ya uongozi wa Mungu, waendeleo kukua na kusonga mbele, kukua na kusonga mbele.

Wakati uliopita, tulijadili kuhusu wazo la msingi la Mungu kuruzuku vitu vyote: Mungu kwanza huvipa vitu vyote kwa njia hii ili vitu vyote viwepo na kuishi kwa ajili ya wanadamu. Yaani, mazingira kama haya yapo kwa ajili ya sheria zilizotungwa na Mungu. Ni tu kwa Mungu kudumisha na kusimamia sheria kama hizi ndio wanadamu wana mazingira ya kuishi waliyonayo sasa. Tulichozungumzia wakati uliopita ni hatua kubwa kutoka kwa ufahamu wa Mungu tuliozungumzia awali. Kwa nini hatua kama hiyo ipo? Kwa sababu tulipozungumzia hapo awali kuhusu kuanza kumjua Mungu, tulikuwa tunajadili katika eneo la Mungu kuwaokoa na kuwasimamia wanadamu—yaani, uokoaji na usimamizi wa watu waliochaguliwa na Mungu—kuhusu kumjua Mungu, matendo ya Mungu, tabia Yake, kile Anacho na Alicho, makusudi Yake, na vile Anampa mwanadamu ukweli na uhai. Lakini mada tuliyozungumza kuhusu wakati uliopita haikujikita tu katika mipaka ya Biblia na katika eneo la Mungu kuwaokoa watu Wake waliochaguliwa. Badala yake, ilitoka nje ya eneo hili, nje ya Biblia, na nje

ya mipaka ya hatua tatu za kazi ambayo Mungu anafanya kwa watu Wake waliochaguliwa na kujadili Mungu Mwenyewe. Hivyo basi ukisikia sehemu hii ya mawasiliano Yangu, lazima usiwekee mipaka ufahamu wako wa Mungu kwa Biblia na hatua tatu za kazi ya Mungu. Badala yake, unahitaji kuuweka wazi mtazamo wako; unahitaji uone matendo ya Mungu na kile Anacho na alichio miongoni mwa vitu vyote, na vile Mungu anatawala na kusimamia vitu vyote. Kupitia kwa mbinu hii na juu ya msingi huu, unaweza kuona vile Mungu anapeana vitu vyote. Hii inawawezesha wanadamu kuelewa kwamba Mungu ni chanzo halisi cha uhai kwa vitu vyote na kwamba huu ni utambulisho halisi wa Mungu Mwenyewe. Hiyo ni kusema, utambulisho wa Mungu, hadhi na mamlaka na kila kitu Chake havilengwi tu kwa wale wanaomfuata Yeye wakati huu—havilengwi tu kwa kundi hili la watu—bali kwa vitu vyote. Basi eneo la vitu vyote ni pana sana. Ninatumia “vitu vyote” kueleza eneo la utawala wa Mungu juu ya vitu vyote kwa sababu Ninataka kuwaambia kwamba vitu vinavyotawaliwa na Mungu si vile mnavyoweza tu kuona kwa macho yenu, bali vinahusisha ulimwengu yakinifu ambao watu wote wanaweza kuuona, na vilevile ulimwengu mwingine usioweza kuonekana kwa macho ya binadamu nje ya ulimwengu yakinifu, na zaidi unahusisha anga na sayari nje ya mahali ambapo wanadamu wapo sasa. Hilo ni eneo la utawala wa Mungu juu ya vitu vyote. Eneo la utawala wa Mungu juu ya vitu vyote ni pana zaidi. Kwenu ninyi, mnachopaswa kuelewa, mnachopaswa kuona, na kutoka kwa vitu mnavyopaswa kupata maarifa—hivi ndivyo kila mmoja wenu anahitaji na ni lazima aelewe, aone, na awe na hakika navyo. Ingawa eneo la hivi “vitu vyote” ni pana, Sitawaambia kuhusu eneo msiloweza kuona kabisa au msiloweza kukutana nalo. Nitawaambia tu kuhusu eneo ambalo binadamu wanaweza kukutana nalo, wanaweza kuelewa, na wanaweza kufahamu, ili kila mmoja aweze kuhisi maana halisi ya kirai hiki “Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote.” Hivyo, chochote Ninachowasilisha kwenu hakitakuwa maneno matupu.

Wakati uliopita, tulitumia mbinu ya kuhadithia ili kutoa maelezo rahisi ya jumla ya mada hii “Mungu Ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote,” ili muwe na ufahamu wa msingi wa jinsi Mungu huvipa vitu vyote. Ni nini kusudi la kuwafundisha kidogokidogo wazo hili la msingi? Ni kuwafanya mjue kwamba, nje ya Biblia na hatua tatu za kazi Yake, Mungu pia anafanya hata kazi nyingi zaidi ambayo wanadamu hawawezi kuona au kukutana nayo. Kazi kama hiyo inatendwa binafsi na Mungu. Kama Mungu angekuwa anaongoza tu watu Wake waliochaguliwa kwenda mbele, bila hii kazi iliyo nje ya kazi Yake ya usimamizi, basi ingekuwa vigumu sana kwa binadamu hawa, ikiwemo pamoja na ninyi nyote, kuendelea kusonga mbele, na binadamu hawa na ulimwengu huu haungeweza kuendelea kukua. Huo ndio umuhimu wa kirai hiki “Mungu Ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote” Ninachowasilisha kwenu siku hii.

Mazingira ya Kuishi ya Msingi Ambayo Mungu Anawaambia Wanadamu

Tumejadili mada nyingi na maudhui yanayohusiana na kirai hiki “Mungu Ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote,” lakini mnajua ndani ya mioyo yenu ni vitu vipi Mungu anatoa kwa wanadamu mbali na kuwapa ninyi neno Lake na kutenda kazi Yake ya kuadibu na hukumu kwenu? Watu wengine huenda wakasema, “Mungu hunipa neema na baraka; Yeye hunifundisha nidhamu na kunifariji na Hunipa utunzaji na ulinzi kwa kila njia iwezekanayo.” Wengine watasema, “Mungu hunipa chakula cha kila siku na kinywaji,” ilhali wengine hata watasema, “Mungu hunipa kila kitu.” Kuhusu vitu hivi ambavyo watu wanaweza kukutana navyo katika maisha yao ya kila siku, nyote mnaweza kuwa na majibu yanayohusiana na matukio mnayopitia katika maisha yenu ya kimwili. Mungu humpa kila mtu mmoja vitu vingi, ingawa tunachojadili leo hakijawekewa mipaka katika eneo la mahitaji ya watu ya kila siku, lakini kinanuiwa kupanua mtazamo wa kila mmoja wenu na kuwawezesha kuona vitu kutoka mbali zaidi. Kwa sababu Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote, Anadumisha vipi uhai wa vitu vyote? Kwa maneno mengine, ni nini ambacho Mungu huleta kwa vitu vyote ili kudumisha kuwepo kwa vitu hivyo na kudumisha sheria za kuwepo kwa vitu hivyo? Hilo ndilo wazo kuu la kile tunachojadili leo. Je, mnaelewa Nilichosema? Mada hii huenda ikawa msiyoifahamu sana, lakini Sitazungumza kuhusu mafundisho ya dini yoyote ambayo ni ya kina sana. Nitajitahidi kuwafanya nyote muelewe baada ya kusikiliza. Hamhitaji kuhisi mzigo wowote—mnachotakiwa kufanya tu ni kusikiliza kwa makini. Kwa hali yoyote, bado Ninahitaji kuisisitiza zaidi kidogo: Ninazungumza juu ya mada gani? Niambieni. (Mungu Ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote.) Basi ni vipi ambavyo Mungu huvipa vitu vyote? Ni nini ambacho Yeye huvipa vitu vyote ili isemwe kwamba “Mungu Ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote”? Je, mna dhana ama mawazo yoyote kuhusu hili? Inaonekana kwamba mada hii Ninayozungumzia kimsingi haileti kinachotumainiwa ndani ya mioyo yenu na ndani ya akili zenu. Lakini Natumai mtaweza kuunganisha mada hii pamoja na vitu Ninavyoenda kuzungumzia kwa matendo ya Mungu, na sio kuviunganisha kwa ufahamu wowote au kuvihusisha na desturi zozote za binadamu au uchunguzi. Ninazungumza tu kuhusu Mungu na kuhusu Mungu Mwenyewe. Hilo ni pendekezo Langu kwenu. Unaelewa, sivyo?

Mungu ametoa vitu vingi kwa wanadamu. Nitaanza kwa kuzungumza kuhusu kile ambacho watu wanaweza kuona, yaani, wanachoweza kuhisi. Hivi ni vitu ambavyo watu wanaweza kuvielewa na wanaweza kukubali. Hivyo basi kwanza tuanze na ulimwengu yakinifu kujadili kile ambacho Mungu amewapa wanadamu.

1. Hewa

Kwanza, Mungu aliumba hewa ili mwanadamu aweze kupumua. Hewa ni chembechembe ambayo kwayo wanadamu wanaweza kuwasiliana nila siku na ni kitu ambacho kwacho

wanadamu hutegemea mara kwa mara, hata wanapolala. Hewa ambayo Mungu aliumba ina umuhimu mkubwa sana kwa wanadamu: ni kijenzi muhimu cha kila pumzi yao na cha uhai wenyewe. Kiini hiki, kinachoweza tu kuhisiwa lakini hakionekani, kilikuwa zawadi ya Mungu ya kwanza kwa vitu vyote. Baada ya kuumba hewa, je, Mungu aliacha kufanya kazi? Baada ya kuumba hewa, je, Mungu alizingatia uzito wa hewa? Je, Mungu alizingatia yaliyomo kwenye hewa? (Ndio.) Mungu alikuwa anafikiria nini alipoumba hewa? Kwa nini Mungu aliumba hewa, na fikira Yake ilikuwa gani? Wanadamu wanahitaji hewa, na wanahitaji kupumua. Kwanza kabisa, uzito wa hewa unapaswa kuwa unaofaa mapafu ya binadamu. Kuna yeyote anayejua uzito wa hewa? Hili si jambo ambalo watu wanahitaji kujua; hakuna haja ya kujua hili. Hatuhitaji idadi kamili kuhusiana na uzito wa hewa, na kuwa na wazo la jumla ni vizuri. Mungu aliumba hewa yenye uzito ambao ungefaa zaidi mapafu ya mwanadamu kupumua. Yaani, wanadamu wanafurahia na haiwezi kudhuru mwili wanapoivuta. Hili ndilo wazo kuhusu uzito wa hewa. Basi tutaongea kuhusu yaliyomo kwenye hewa. Kwanza, yaliyomo ndani ya hewa si sumu kwa wanadamu na hivyo hayata dhuru pafu na mwili. Mungu alihitaji kuzingatia haya yote. Mungu alihitaji kuzingatia kwamba hewa ambayo wanadamu wanapumua inapaswa kuingia na kutoka taratibu, na kwamba, baada ya kuvuta hewa, kadiri na kiasi cha hewa vinapaswa kuhakikisha damu pamoja na hewa chafu ndani ya mapafu na mwili vingejenga na kuvunjavunja kemikali mwilini vizuri, na pia kwamba hewa hiyo haipaswi kuwa na vijenzi vyovyote vya sumu. Kuhusu viwango hivi viwili, Sitaki kuwalisha mafungu ya maarifa, lakini badala yake nataka tu mjue kwamba Mungu alikuwa na mchakato maalum wa mawazo akilini mwake Alipoumba kila kitu—bora zaidi. Aidha, kuhusu kiasi cha vumbi katika hewa, kiasi cha vumbi, mchanga na uchafu duniani, na vilevile vumbi inayoelekea chini kutoka angani, Mungu alikuwa na mpango wa vitu hivi pia, njia za kuviondoa ama kuvisababisha vivunjike. Huku kukiwa na vumbi kiasi, Mungu aliumba ili vumbi isidhuru mwili na upumuaji wa mwanadamu, na kwamba vipande vya vumbi viwe na ukubwa usiokuwa na madhara kwa mwili. Je, uumbaji wa Mungu wa hewa haukuwa wa ajabu? Je, ulikuwa rahisi kama kupuliza pumzi ya hewa kutoka kinywani Mwake? (La.) Hata katika uumbaji wake wa vitu rahisi sana, maajabu ya Mungu, akili Zake, mawazo Yake, na hekima Yake vyote ni dhahiri. Je, Mungu si mwenye vitendo? (Ndiyo, yeye Ndiye). Maana ya hii ni kwamba, hata katika kuumba vitu rahisi, Mungu alikuwa akifikiria kuhusu mwanadamu. Kwanza kabisa, hewa ambayo wanadamu hupumua ni safi, yaliyomo yanafaa kwa upumuaji wa mwanadamu, si sumu na hayasababishi madhara kwa wanadamu, na uzito huo umekadiriwa kwa upumuaji wa wanadamu. Hewa hii ambayo wanadamu huvuta pumzi na kutoa ni muhimu kwa mwili wao, umbo lao. Ili wanadamu waweze kupumua kwa uhuru, bila kizuizi au wasiwasi. Waweze kupumua kwa kawaida. Hewa ni kile ambacho Mungu aliumba mwanzo na ambacho ni cha lazima kwa upumuaji wa wanadamu.

2. Halijoto

Kitu cha pili ni halijoto. Kila mtu anajua halijoto ni nini. Halijoto ni kitu ambacho mazingira yanayofaa kuishi kwa wanadamu ni lazima yawe nacho. Ikiwa halijoto iko juu sana, tuseme ikiwa halijoto iko juu zaidi ya nyuzi Selisiasi 40, basi haingekuwa inachosha sana kwa wanadamu? Je, haingekuwa inachosha kwao kuishi? Je, na halijoto ikiwa chini sana, na kufikia nyuzi hasi Selisiasi 40? Wanadamu hawataweza pia kuistahimili. Kwa hiyo, Mungu alikuwa mwangalifu sana katika kuviweka vipimo hivi vya halijoto. Vipimo vya halijoto ambavyo mwili wa mwanadamu unaweza kufanya mabadiliko kimsingi ni nyuzi hasi Selisiasi 30 hadi nyuzi Selisiasi 40. Hiki ndicho kipimo cha halijoto cha msingi kutoka kaskazini mpaka kusini. Katika maeneo ya baridi, halijoto inaweza kuteremka mpaka nyuzi hasi 50 hadi 60 Selisiasi. Eneo kama hilo si mahali ambapo Mungu anamruhusu mwanadamu kuishi. Mbona kuna maeneo ya baridi hivyo? Katika hayo kuna hekima na makusudi ya Mungu. Hakuruhusu kusonga karibu na sehemu hizo. Mungu hulinda sehemu zilizo na joto sana na baridi sana, kumaanisha Hayuko tayari kumruhusu mwanadamu kuishi huko. Si kwa wanadamu. Kwa nini akaruhusu sehemu kama hizo kuwepo duniani? Ikiwa Mungu hangemruhusu mwanadamu kuishi au kuwepo huko, basi kwa nini akaziumba? Hekima ya Mungu imo humo. Yaani, halijoto ya msingi ya mazingira ya kuendelea kuishi kwa mwanadamu pia imerekebisha na Mungu vya kutosha. Kuna sheria hapa pia. Mungu aliumba vitu vingine kusaidia kudumisha halijoto kama hiyo, kudhibiti halijoto hiyo. Ni vitu gani vinatumiwa kudumisha halijoto hii? Kwanza kabisa, jua linaweza kuwaletea watu uvuguvugu, lakini watu wataweza kustahimili iwapo ni vuguvugu sana? Je, kuna yeyote anaweza thubutu kukaribia jua? Je, kuna kifaa chochote duniani kinachoweza kusonga karibu na jua? (La.) Mbona? Ni joto sana. Kitayeyuka kikaribiapo jua. Kwa hiyo, Mungu ametengeneza kipimo maalum cha umbali wa jua kutoka kwa wanadamu: Amefanya kazi maalumu. Mungu ana kiwango cha umbali huu. Vilevile kuna Ncha ya kusini na Ncha ya Kaskazini za dunia. Kote huko kuna mito ya barafu. Wanadamu wanaweza kuishi juu ya mito ya barafu? Inafaa kuishi kwa wanadamu? (La.) La, hivyo watu hawataenda huko. Kwa vile watu hawaendi katika Ncha za Kusini na Kaskazini, mito ya barafu itahifadhiwa, na itaweza kufanya wajibu wake, ambao ni kudhibiti halijoto. Unaelewa? Ikiwa hakuna Ncha za Kusini na Kaskazini na jua linawaka juu ya dunia kila wakati, basi watu wote juu ya dunia watakufa kutokana na joto. Je, Mungu hutumia tu vitu hivi viwili kudhibiti halijoto inayofaa kuishi kwa wanadamu? La, pia kuna kila aina za viumbe vyenye uhai, kama vile nyasi juu ya mbuga za malisho, aina mbalimbali za miti na kila aina ya mimea iliyo ndani ya misitu vinafyonza joto la jua na kwa kufanya hivyo, vinabatilisha nishati ya joto ya jua kwa njia inayorekebisha halijoto ya mazingira ambamo wanadamu wanaishi. Pia kuna vyanzo vya maji, kama vile mito na maziwa. Sehemu ya juu ya mito na maziwa si kitu kinachoweza kuamuliwa na yeyote. Hakuna yeyote anayeweza kudhibiti kiasi cha

maji yaliyo juu ya dunia, wapi maji hayo yanatiririka, mwelekeo wa kutiririka huko, wingi wa maji hayo, au spidi ya mtiririko huo. Mungu pekee ndiye ajuaye. Vyanzo hivi mbalimbali vya maji, yakiwemo maji ya chini ya ardhi na mito na maziwa yaliyo juu ya ardhi ambayo watu wanaweza kuona, yanaweza pia kurekebisha halijoto ambayo wanadamu wanaishi ndani. Zaidi ya hayo, kuna kila aina ya uumbaji wa kijiografia, kama vile milima, tambarare, korongo kuu na ardhi ya majimaji wa uumbaji huu mbalimbali wa kijiografia na sehemu zao za juu na ukubwa vyote vina umuhimu katika kudhibiti halijoto. Kwa mfano, ikiwa mlima una mzinga wa kilomita mia moja, kilomita hizi 100 zitakuwa na athari ya kilomita 100. Lakini kuhusu safu za milima na korongo kuu ngapi kama hizo ambazo Mungu ameumba juu ya dunia, hili ni jambo ambalo Mungu amelifikiria kabisa. Kwa maneno mengine, nyuma ya kuwepo kwa kila kitu kilichoumbwa na Mungu kuna hadithi, na pia kina hekima na mipango ya Mungu. Tuseme, kwa mfano, misitu na kila aina mbalimbali za mimea—safu na ukubwa wa eneo ambamo vinapatikana na kukua haudhibitiwi na mwanadamu yeyote na hakuna anayetawala vitu hivi. Kiasi cha maji ambayo vinafyonza, kiasi cha nishati ya joto ambayo vinafyonza kutoka kwa jua pia haviwezi kudhibitiwa na mwanadamu yeyote. Vitu hivi vyote viko katika eneo la kile kilichopangwa na Mungu alipoumba vitu vyote.

Ni kwa sababu tu ya upangaji wa makini, fikira, na utaratibu wa Mungu katika vipengele vyote ndio mwanadamu anaweza kuishi katika mazingira yaliyo na halijoto ya kufaa hivyo. Kwa hiyo, kila kitu ambacho mwanadamu anakiona kwa macho yake, kama vile jua, Ncha za Kusini na Kaskazini ambazo watu mara nyingi husikia kuzihusu, vilevile viumbe mbalimbali vilivyo hai juu na chini ya ardhi na ndani ya maji, na sehemu za juu zenye misitu na aina zingine za mimea, na vyanzo vya maji, mikusanyiko mbalimbali ya maji, kuna kiasi gani cha maji chumvi na maji baridi, kuongezea mazingira mbalimbali ya kijiografia—Mungu hutumia vitu hivi kudumisha halijoto ya kawaida kwa kuishi kwa mwanadamu. Hii ni thabiti. Ni kwa sababu tu Mungu ana fikira kama hizi ndio mwanadamu anaweza kuishi katika mazingira yaliyo na halijoto ya kufaa hivyo. Haiwezi kuwa baridi zaidi wala joto zaidi: sehemu zenye joto zaidi na ambapo halijoto inazidi kile ambacho mwili wa mwanadamu unaweza kuzoea bila shaka hazijatayarishwa na Mungu kwa ajili yako. Sehemu zenye baridi zaidi na ambapo halijoto ni ya chini zaidi; sehemu ambazo, punde tu wanadamu wanapowasili, zitawafanya wagande sana baada ya dakika chache mpaka wasiweze kuzungumza, ubongo wao utaganda, wasiweze kufikiri, na hatimaye watakosa hewa—sehemu kama hizo pia hazijatayarishwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu. Haijalishi ni aina gani ya uchunguzi wanadamu wanataka kufanya, au kama wanataka kuvumbua au wanataka kutengua mipaka hiyo—haijalishi watu wanafikiria nini, hawataweza kamwe kuzidi mipaka ya kile ambacho mwili wa mwanadamu unaweza kuzoea. Hawataweza kuondoa mipaka hiyo ambayo Mungu alimuambia mwanadamu. Hii ni kwa sababu Mungu aliwaumba wanadamu, na

Mungu anajua bora zaidi ni halijoto gani mwili wa mwanadamu unaweza kuzoea. Lakini wanadamu wenyewe hawajui. Mbona nasema wanadamu hawajui? Ni mambo gani ya upumbavu ambayo wanadamu wamefanya? Je, hakujakuwa na watu wachache ambao kila mara wanataka kushindana na Ncha za Kaskazini na Kusini? Watu kama hao daima wametaka kwenda kwenye sehemu hizo kumiliki ardhi hiyo, ili waweze kujisitawisha huko. Hiki kingekuwa kitendo cha upumbavu. Hata iwapo umechunguza kikamilifu pembe za dunia, halafu nini? Hata iwapo unaweza kuzoea joto na una uwezo wa kuishi hapo, ingeweza kumfaa mwanadamu kwa njia yoyote iwapo “ungeboresha” hali ya sasa ya maisha katika Ncha za Kusini na Kaskazini? Wanadamu hawana mazingira ambayo kwayo wanaweza kuendelea kuishi ndani, lakini wanadamu hawabaki hapo kwa ukimya na utiifu, ila badala yake wanasisitiza kuenda maeneo ambapo hawawezi kuishi. Kwa nini ni hivyo? Wamechoshwa na kuishi katika halijoto hii ya kufaa. Wamefurahia baraka nyingi sana. Mbali na hayo, haya mazingira ya kuishi ya kawaida yameharibiwa kiasi sana na wanadamu, hivyo wanaweza basi kwenda kwa Ncha ya Kusini na Ncha ya Kaskazini ili wafanye madhara mengi zaidi au kujihusisha katika “kusudi,” fulani ili waweze kuwa “watangulizi” wa aina fulani. Si huu ni upumbavu? Hivyo ni kusema, chini ya uongozi wa babu yao Shetani, wanadamu hawa wanaendelea kufanya kitu kimoja cha upuuzi baada ya kingine, wakiharibu bila hadhari na kwa utukutu makao mazuri ambayo Mungu aliwaambia wanadamu. Hili ndilo Shetani alifanya. Zaidi ya hayo, kwa kuona kwamba kuendelea kuishi kwa wanadamu duniani kuko katika hatari kidogo, watu wengi sana wanataka kutafuta njia za kwenda kuishi juu ya mwezi, kutafuta njia ya kuondoka kwa kuona ikiwa wanaweza kuishi huko. Hatimaye, inakosekana kwenye mwezi. Je, wanadamu wanaweza kuendelea kuishi bila oksijeni? Kwa vile mwezi hauna oksijeni, si mahali ambapo mwanadamu anaweza kuishi huko, ilhali mwanadamu anaendelea kutaka kwenda huko. Hii ni nini? Ni kujiangamiza, sivyo? Ni mahali pasipo na hewa, na halijoto haifai kwa kuendelea kuishi kwa mwanadamu, hivyo hapajatayarishwa na Mungu kwa ajili ya mwanadamu.

Mada yetu sasa hivi, halijoto ni kitu ambacho watu hukutana nacho katika maisha yao ya kila siku. Halijoto ni kitu ambacho miili yote ya wanadamu inaweza kuhisi, lakini hakuna anayefikiria vile halijoto hii iliumbwa, au ni nani anasimamia na kudhibiti halijoto ya kufaa kuishi kwa wanadamu. Hiki ndicho tunaanza kujua sasa. Je, kuna hekima ya Mungu katika hili? Je, kuna kitendo cha Mungu katika hili? (Ndiyo.) Ukifikiria kwamba Mungu aliumba mazingira yenye halijoto ya kufaa kuishi kwa wanadamu, je, hii ni njia moja ambayo Mungu huvipa vitu vyote? (Ndiyo.) Ni kweli.

3. Sauti

Kitu cha tatu ni nini? Pia ni kitu ambacho mazingira ya kuishi ya kawaida ya wanadamu

yanatakiwa kuwa nacho. Ni kitu ambacho Mungu alishughulikia alipoumba vitu vyote. Hiki ni kitu muhimu sana kwa Mungu na pia kwa kila mtu. Kama Mungu hakushughulikia suala hilo, ingekuwa kizuizi kikubwa kwa kuendelea kuishi kwa wanadamu. Hiyo ni kusema kwamba ingekuwa na athari yenye maana sana kwa mwili na maisha ya mwanadamu, kiasi kwamba wanadamu hawangeweza kuendelea kuishi katika mazingira kama hayo. Pia inaweza kusemwa kwamba viumbe vyote vyenye uhai haviwezi kuendelea kuishi katika mazingira kama hayo. Hivyo hiki ni kitu gani? Ni sauti. Mungu aliumba kila kitu, na kila kitu kinaishi mikononi mwa Mungu. Machoni pa Mungu, vitu vyote vinasonga na vinaishi. Yaani kuwepo kwa kila mojawapo ya vitu vilivyoumbwa na Mungu kuna thamani na maana. Yaani, vyote vina umuhimu katika kuwepo kwao. Kila kitu kina uhai machoni pa Mungu; kwa kuwa vyote viko hai, vitatoa sauti. Kwa mfano, dunia daima inazunguka, jua daima linazunguka, na mwezi daima unazunguka pia. Sauti daima zinatolewa katika uzalishaji na kuendelea na miendo ya vitu vyote. Vitu juu ya dunia daima vinazaa, kukua na kusonga. Kwa mfano, misingi ya milima inasonga na kubadilisha nafasi, na vitu vyote vyenye uhai katika kina cha bahari vinasonga na kuogelea na kwenda hapa na pale. Hii inamaanisha kwamba vitu hivi vyenye uhai, vitu vyote anavyoviona Mungu, vyote viko mara kwa mara, kwa mwendo wa kawaida, kulingana na mifumo iliyoanzishwa. Kwa hivyo, ni nini kinaletwa na uzalishaji wa siri na maendeleo na miendo ya vitu hivyo? Sauti za nguvu. Mbali na dunia, kila aina ya sayari daima ziko katika mwendo, na viumbe vyenye uhai na viumbe hai juu ya sayari hizo pia daima vinazaa, vinakua na viko katika mwendo. Yaani, vitu vyote vilivyo na uhai na visivyo na uhai daima vinasonga mbele machoni pa Mungu, na pia vinatoa sauti wakati huo huo. Mungu pia ameshughulikia sauti hizi. Mnapaswa kujua sababu ya mbona sauti hizi zinashughulikiwa, sivyo? Unaposonga karibu na ndege, sauti ya kunguruma ya ndege itakufanyia nini? Masikio yako yatazibwa muda unavyozidi kusonga. Je, mioyo yenu itaweza kuistahimili? Wengine wenye mioyo hafifu hawataweza kuistahimili. Bila shaka, hata wale wenye mioyo yenye nguvu hawataweza kuistahimili ikiendelea kwa muda mrefu. Hiyo ni kusema, athari ya sauti kwa mwili wa mwanadamu, kama ni kwa masikio au moyo, ni yenye maana kabisa kwa kila mtu, na sauti ambazo ni za juu sana zitaleta madhara kwa watu. Kwa hiyo, Mungu alipoumba vitu vyote na baada ya hivyo kuanza kufanya kazi kwa kawaida, Mungu pia aliweka sauti hizi—sauti za vitu vyote vilivyo katika mwendo—kupitia kwa utendeaji wa kufaa. Hii pia ni mojawapo ya fikira muhimu alizokuwa nazo Mungu alipoumbia wanadamu mazingira.

Kwanza kabisa, kimo cha angahewa kutoka kwa uso wa dunia kitaathiri sauti. Pia, ukubwa wa utupu ndani ya mchanga, pia utaendesha na kuathiri sauti. Kisha kuna mahali mito miwili inapoungana pa mazingira mbalimbali ya kijiografia, ambapo pia pataathiri sauti. Hiyo ni kusema, Mungu hutumia mbinu fulani kuondoa sauti zingine, ili wanadamu waweze kuendelea

kuishi katika mazingira ambayo masikio na mioyo yao vinaweza kustahimili. La sivyo sauti zitaleta kizuizi kikubwa kwa kuendelea kuishi kwa wanadamu; zitaleta matatizo makubwa kwa maisha yao. Hili litakuwa tatizo kubwa kwao. Hiyo ni kusema, Mungu alikuwa mwenye kujali sana katika uumbaji Wake wa nchi, angahewa, na aina mbalimbali za mazingira ya kijiografia. Hekima ya Mungu iko ndani ya haya yote. Ufahamu wa wanadamu kuhusu haya hauhitaji kuwa kinaganaga sana. Kila wanachohitaji kujua ni kwamba kitendo cha Mungu kimo humo. Sasa Niambieni, hii kazi ambayo Mungu alifanya ilikuwa muhimu? Yaani, uendeshaji wa taratibu sana wa sauti ili kudumisha mazingira ya kuishi ya wanadamu na maisha yao ya kawaida. (Ndiyo.) Ikiwa kazi hii ilikuwa muhimu, basi kutokana na mtazamo huu, je, inaweza kusemwa kwamba Mungu alitumia mbinu kama hii kupeana vitu vyote? Mungu aliwapa wanadamu na kuumba mazingira haya tulivu, ili kwamba mwili wa mwanadamu uweze kuishi kwa kawaida kabisa katika mazingira haya bila vizuizi vyovyote, na ili kwamba mwanadamu ataweza kuwepo na kuishi kwa kawaida. Je, hii si njia mojawapo ambayo kwayo Mungu huwapa wanadamu? Je, jambo hili alilofanya Mungu lilikuwa muhimu sana? (Ndiyo.) Lilikuwa muhimu sana. Je, ni vipi ambavyo mnashukuru hili? Hata kama hamwezi kuhisi kwamba hiki kilikuwa kitendo cha Mungu, wala hamjui vile Mungu alikifanya wakati huo, je, bado mnaweza kuhisi umuhimu wa Mungu kufanya hilo? Je, mnaweza kuhisi hekima ya Mungu au umakini na wazo Aliyoweka katika jambo hili? (Ndiyo.) Kuweza tu kuhisi hili ni sawa. Yatosha. Kuna vitu vingi ambavyo Mungu amefanya miongoni mwa vitu vyote ambavyo watu hawawezi kuhisi na kuona. Lengo la Mimi kukitaja hapa ni kuwapa tu habari kiasi kuhusu matendo ya Mungu ili muweze kuanza kumjua Mungu. Vidokezo hivi vinaweza kuwafanya mjue na kumwelewa Mungu vizuri zaidi.

4. Nuru

Kitu cha nne kinahusiana na macho ya watu—nacho ni, nuru. Hiki pia ni muhimu sana. Unapoona nuru inayong'aa, na mwangaza wa nuru hiyo ukafikia kiasi fulani, macho yako yatapofushwa. Hata hivyo, macho ya wanadamu ni macho ya mwili. Hayawezi kustahimili kuwashwa. Je, kuna yeyote anayethubutu kulitazama jua moja kwa moja? Watu wengine wamejaribu. Unaweza kutazama ukiwa umevaa miwani ya jua, sivyo? Hilo linahitaji usaidizi wa vifaa. Bila vifaa, macho makavu ya mwanadamu hayathubutu kutazama jua moja kwa moja. Hata hivyo, Mungu aliumba jua ili awape wanadamu nuru, na pia aliendesha nuru hii. Mungu hakuliacha tu jua na kulipuuza baada ya kuliumba. “Nani anajali iwapo macho ya mwanadamu yanaweza kulistahimili!” Mungu hafanyi vitu hivyo. Yeye hufanya vitu kwa uangalifu sana na huzingatia vipengele vyote. Mungu aliwapa wanadamu macho ili waweze kuona, lakini Mungu ametayarisha pia umbali wa mwangaza ambao wanaweza kutazama chini yake. Haitawezekana iwapo hakuna nuru ya kutosha. Iwapo kuna giza sana mpaka watu hawawezi kuona mkono wao ulio mbele yao, kisha macho yao yatapoteza kazi yake na hayatakuwa na faida yoyote. Sehemu

iliyo na mwangaza mwingi itakuwa haivumiliki kwa macho ya mwanadamu na pia hawataweza kuona chochote. Hivyo katika mazingira wanayoishi ndani wanadamu, Mungu amewapa kiasi cha nuru kinachofaa macho ya wanadamu. Nuru hii haitaumiza wala kudhuru macho ya watu. Zaidi ya hayo, haitayafanya macho ya watu yapoteze matumizi yake. Hii ndiyo sababu ambayo Mungu aliongeza mawingu yanayozunguka jua na dunia, na uzito wa hewa unaweza pia kuchuja kwa kawaida nuru inayoweza kuumiza macho ya watu au ngozi. Haya yanahusiana. Kuongezea, rangi ya dunia iliyumbwa na Mungu huakisi pia nuru ya jua na kuondoa ile sehemu ya mwangaza katika nuru inayofanya macho ya wanadamu kutokuwa na raha. Kwa njia hiyo, watu hawahitaji kila mara kuvaa miwani myeusi sana ya jua ili waweze kutembea huko nje na kufanya shughuli za maisha yao. Katika hali za kawaida, macho ya wanadamu yanaweza kuona vitu vilivyo katika eneo la kuona kwao na hayataingiliwa kati na nuru. Yaani, nuru hii haiwezi kuwa ya kuchoma sana wala ya kufifiliza, ikiwa ya kufifiliza sana, macho ya watu yatadhuriwa na hawataweza kuyatumia kwa muda mrefu sana kabla ya macho yao kuacha kutumika; ikiwa ina mwangaza sana, macho ya watu hayataweza kuistahimili. Nuru ii hii ambayo watu wanayo inapaswa iwe ya manufaa kwa macho ya wanadamu kuona, na madhara yanayoletwa kwa macho ya wanadamu na nuru yamepunguzwa na Mungu kupitia kwa mbinu mbalimbali. Haijalishi ikiwa nuru huleta faida au kikwazo kwa macho ya wanadamu, inatosha kuyawezesha macho ya watu kuendelea kuishi mpaka mwisho wa maisha yao. Je, Mungu hajalifikiria hilo kikamilifu sana? Lakini wakati Shetani, ibilisi, anafanya mambo, hafikirii mambo haya. Nuru hiyo ama ina mwangaza sana au inafifiliza sana Hivi ndivyo Shetani hufanya vitu.

Mungu alifanya vitu hivi katika vipengele vyote vya mwili wa mwanadamu—kuona, kusikia, kuonja, kupumua, hisia ... kuongeza hadi upeo uwezo wa kubadilisha wa kuendelea kuishi kwa wanadamu ili waweze kuishi kwa kawaida na kuendelea kuishi. Yaani ni kusema, mazingira ya kuishi kama hayo yaliyopo yaliyumbwa na Mungu ni mazingira ya kuishi yanayofaa zaidi na yenye faida kwa kuendelea kuishi kwa wanadamu. Wengine wanaweza kufikiri kwamba hii haitoshi na kwamba yote ni ya kawaida sana. Sauti, nuru, na hewa ni vitu ambavyo watu hufikiria kwamba walizaliwa navyo, vitu wanavyoweza kufurahia tangu wakati wa kuzaliwa. Lakini kile alichofanya Mungu kinachosababisha kufurahia kwao kwa vitu hivi ni kitu wanachohitaji kujua na kuelewa. Haijalishi ikiwa unahisi kuna haja ya kuelewa au kujua vitu hivi, kwa ufupi, Mungu alipoumba vitu hivi, alikuwa ametumia fikira, Alikuwa na mpango, Alikuwa na mawazo fulani. Hakuwaweka wanadamu katika mazingira ya kuishi kama haya kwa kawaida, kwa bahati, au bila kufikiria. Huenda mkadhani kwamba Nimezungumza kwa kwa fahari kuhusu vitu hivi vyote vidogo, lakini kwa mtazamo Wangu, kila kitu ambacho Mungu aliwapa wanadamu ni muhimu kwa kuendelea kuishi kwa binadamu. Kuna tendo la Mungu katika hili.

5. Bubujiko la Hewa

Kitu cha tano ni kipi? Kitu hiki kinahusiana sana na kila siku ya mwanadamu, na uhusiano huu thabiti. Ni kitu ambacho mwili wa mwanadamu hauwezi kuishi bila katika ulimwengu huu yakinifu. Kitu hiki ni bubujiko la hewa. “Bubujiko la hewa” ni neno ambalo watu wote labda wanaelewa. Hivyo bubujiko la hewa ni nini Mngesema kwamba kububujika kwa hewa kunaitwa “bubujiko la hewa.” Bubujiko la hewa ni upepo ambao jicho la mwanadamu haliwezi kuona. Pia ni njia ambayo gesi husonga. Lakini ni bubujiko la hewa gani tunalozungumzia hapa? Mtaelewa punde Nitakaposema. Dunia hubeba milima, bahari, na vitu vyote inapogeuka, na inapogeuka kuna spidi. Hata ikiwa huwezi kuhisi kuzunguka kokote, mzunguko wake upo kweli. Mzunguko wake huleta nini? Huwa kuna upepo kando ya masikio yako unapokimbia? Ikiwa upepo unaweza kuzalishwa unapokimbia, inawezekanaje kutokuwepo kwa nguvu za upepo dunia inapozunguka? Dunia inapozunguka, vitu vyote viko katika mwendo. Iko katika mwendo na kuzunguka katika spidi fulani, wakati vitu vyote duniani daima vinazaa na kukua. Kwa hiyo, kusonga kwa spidi fulani kwa kawaida kutaleta bubujiko la hewa. Hilo ndilo bubujiko la hewa. Bubujiko la hewa hilo litaathiri mwili wa mwanadamu kwa kiasi fulani? Unaona, tufani za kawaida hazina nguvu sana, lakini zinapotokea, watu hawawezi kusimama kwa utulivu na huona vigumu kutembea katika upepo huo. Ni vigumu hata kutembea hatua moja. Ina nguvu sana, baadhi ya watu wanasukumwa na upepo dhidi ya kitu na hawawezi kusonga. Hii ni mojawapo ya njia ambazo bubujiko la hewa linaweza kuathiri wanadamu. Ikiwa dunia nzima ingekuwa imejaa tambarare, ingekuwa vigumu mno kwa mwili wa binadamu kuhimili bubujiko la hewa ambalo lingezalishwa na mzunguko wa dunia na mwendo wa vitu vyote katika spidi fulani. Ingekuwa vigumu zaidi kustahimili. Ingekuwa hivyo, hili bubujiko la hewa halingeleta tu madhara kwa wanadamu, bali uharibifu. Hakuna ambaye angeweza kuendelea kuishi katika mazingira hayo. Ndio maana Mungu hutumia mazingira mbalimbali ya kijiografia kutatua aina hiyo ya mabubujiko ya hewa—katika mazingira tofauti, mabubujiko ya hewa hufifia, hubadili mwelekeo wake, hubadili kasi yake na hubadili nguvu yake. Ndio maana watu wanaweza kuona mazingira ya jiografia mbalimbali, kama vile milima, safu za milima, tambarare, vilima, vidimbwi, mabonde, uwanda wa juu, na mito. Mungu hutumia haya mazingira mbalimbali ya jiografia kubadilisha spidi, mwelekeo na nguvu za bubujiko la hewa, akitumia mbinu kama hiyo kupunguza au kuiendesha kuwa spidi ya upepo, mwelekeo wa upepo, na nguvu za upepo zinazofaa, ili wanadamu waweze kuwa na mazingira ya kuishi ya kawaida. Je, ni lazima kufanya hivyo? (Ndiyo.) Kufanya jambo kama hilo kunaonekana kuwa vigumu kwa wanadamu, lakini ni rahisi kwa Mungu kwa sababu Anaangalia kwa makini vitu vyote. Kwa Yeye kuumba mazingira yenye bubujiko la hewa linalofaa wanadamu ni kitu sahili sana, rahisi sana. Kwa hiyo, katika mazingira kama hayo yaliyoubwa na Mungu, kila kitu na vitu vyote miongoni mwa vitu vyote

ni vya lazima. Kuna thamani na umuhimu katika kila kuwepo kwa vitu hivyo. Hata hivyo, kanuni hii haieleweki na Shetani au kwa mwanadamu ambaye amepotoshwa. Wanaendelea kuharibu na kukuza, wakiota bure juu ya kugeuza milima kuwa ardhi tambarare, kujaza korongo kuu, na kujenga magorofa juu ya ardhi tambarare kuunda misitu ya saruji. Ni matumaini ya Mungu kwamba wanadamu wataishi kwa furaha, kukua kwa furaha, na kutumia kila siku kwa furaha katika mazingira ya kufaa zaidi Aliyowatayarishia. Ndiyo maana Mungu hajawahi kuwa mzembe inapohusu kushughulikia mazingira ya kuishi ya wanadamu. Kutoka kwa halijoto mpaka kwa hewa, kutoka kwa sauti mpaka kwa nuru, Mungu amefanya mipango na utaratibu tatanishi, ili mazingira ya kuishi ya wanadamu na miili yao visiweze kupatwa na kuharibiwa kokote kutoka kwa hali za asili, na badala yake wanadamu waweze kuishi na kuongezeka kawaida na kuishi na vitu vyote kawaida kwa kuishi pamoja kwa amani yenye kuridhisha. Hii yote inapeanwa na Mungu kwa vitu vyote na wanadamu.

Je, unaweza kuona, kutokana na jinsi Alishughulikia hali hizi tano za msingi za kuendelea kuishi kwa wanadamu, upeanaji wa Mungu kwa wanadamu? (Ndiyo.) Hiyo ni kusema kwamba Mungu aliumba msingi kabisa kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa wanadamu. Wakati huo huo, Mungu pia anasimamia na kudhibiti vitu hivi vyote, na hata sasa, baada ya wanadamu kuwepo kwa maelfu ya miaka, Mungu bado daima anabadilisha mazingira yao ya kuishi, kupeana mazingira ya kuishi yaliyo bora zaidi na ya kufaa zaidi kwa wanadamu ili maisha yao yaweze kudumishwa kwa kawaida. Haya yatadumishwa mpaka lini? Kwa maneno mengine, Mungu ataendelea kupeana mazingira kama haya kwa muda gani? Mpaka Mungu akamilishe kabisa kazi Yake ya usimamizi. Kisha, Mungu atabadilisha mazingira ya kuishi ya wanadamu. Huenda ikawa kupitia kwa mbinu zile zile, au huenda ikawa kupitia kwa mbinu tofauti, lakini kile ambacho watu wanahitaji kujua sasa ni kwamba Mungu daima anapeana mahitaji ya wanadamu, anasimamia mazingira ya kuishi ya wanadamu, na kutunza, kuhifadhi na kudumisha mazingira ya kuishi ya wanadamu. Ni kwa sababu ya mazingira kama hayo ndiyo watu waliochaguliwa na Mungu wanaweza kuishi kwa kawaida hivyo na kukubali wokovu wa Mungu na kuadibu na hukumu. Vitu vyote vinaendelea kuwepo kwa sababu ya kanuni ya Mungu, wakati wanadamu wote wanaendelea kusonga mbele kwa sababu ya upeanaji wa Mungu kwa jinsi hii.

Je, sehemu hii ambayo Nimewasilisha sasa hivi imewaletea mawazo yoyote mapya? Je, sasa mnahisi tofauti kubwa kabisa kati ya Mungu na wanadamu? Nani hasa ndiye bwana wa vitu vyote? Ni mwanadamu? (La.) Basi ni nini tofauti kati ya vile Mungu na wanadamu hushughulikia vitu vyote? (Mungu hutawala na kupanga vitu vyote, ilhali mwanadamu hufurahia vitu hivyo vyote.) Je, mnakubaliana na maneno hayo? Tofauti kubwa kabisa kati ya Mungu na wanadamu ni kwamba Mungu hutawala vitu vyote na hupeana vitu vyote. Mungu ni chanzo cha vitu vyote, na wanadamu hufurahia vitu vyote wakati Mungu anawapa. Hiyo ni kusema,

mwanadamu hufurahia vitu vyote anapokubali maisha ambayo Mungu anatoa kwa vitu vyote. Wanadamu hufurahia matokeo ya uumbaji wa Mungu wa vitu vyote, ilhali Mungu ni Bwana. Kisha kutokana na mtazamo wa vitu vyote, ni nini tofauti kati ya Mungu na wanadamu? Mungu anaweza kuona vizuri mipangilio ya ukuaji wa vitu vyote, na kudhibiti na kutawala mipangilio ya ukuaji wa vitu vyote. Yaani, vitu vyote vipo machoni mwa Mungu na katika eneo Lake la ukaguzi. Je, wanadamu wanaweza kuona vitu vyote? Kile ambacho wanadamu huona kimewekewa mipaka—ni tu kile wanachoonza mbele ya macho yao. Ukiukwea mlima huu, unachoonza ni mlima huu. Huwezi kuona kilicho upande mwingine wa mlima huo. Ukienda pwani, unaweza kuona upande huu wa bahari, lakini hujui upande ule mwingine wa bahari ulivyo. Ukiwasili katika msitu huu, unaweza kuona mimea iliyo mbele ya macho yako na inayokuzunguka, lakini huwezi kuona iliyo mbele zaidi. Wanadamu hawawezi kuona sehemu zilizo juu sana, mbali sana na kina sana. Kile wanachoweza kuona ni kilicho mbele ya macho yao na katika mpaka wa uwezo wao wa kuona. Hata kama wanadamu wanajua mpangilio wa misimu minne katika mwaka na mpangilio wa ukuaji wa vitu vyote, hawawezi kusimamia au kutawala vitu vyote. Kwa upande mwingine, vile Mungu aonavyo vitu vyote ni kama vile Mungu angeona mashine Aliyotengeneza binafsi. Angejua kila kijenzi vizuri kabisa. Kanuni zake ni zipi, mipangilio yake ni ipi, na kusudi lake ni lipi—Mungu anajua vitu hivi vyote wazi na dhahiri. Kwa hiyo Mungu ni Mungu, na mwanadamu ni mwanadamu! Hata mwanadamu akiendelea kuchunguza sayansi na sheria za vitu vyote, ni katika eneo lililowekewa mipaka pekee, ilhali Mungu anadhibiti vitu vyote. Kwa mwanadamu, hiyo ni isiyo na kikomo. Wanadamu wakichunguza kitu fulani kidogo ambacho Mungu alifanya, wangetumia maisha yote kukichunguza bila kupata matokeo yoyote ya kweli. Ndiyo maana ukitumia ufahamu na kile ulichojifunza kumsoma Mungu, hutaweza kamwe kujua au kuelewa Mungu. Lakini ukitumia njia ya kutafuta ukweli na kumtafuta Mungu, na kumtazama Mungu kutokana na mtazamo wa kuanza kumjua Mungu, basi siku moja utakubali kwamba matendo na hekima ya Mungu viko kila mahali, na utajua pia hasa ni kwa nini Mungu huitwa Bwana wa vitu vyote na chanzo cha uhai kwa vitu vyote. Kadiri unavyokuwa na maarifa kama hayo, ndivyo utakavyoelewa ni kwa nini Mungu huitwa Bwana wa vitu vyote. Vitu vyote na kila kitu, pamoja na wewe, daima vinapokea mtiririko thabiti wa upeanaji wa Mungu. Utaweza pia kuhisi dhahiri kwamba katika ulimwengu huu, na miongoni mwa wanadamu hawa, hakuna yeyote isipokuwa Mungu anayeweza kuwa na nguvu kama hizo na kiini kama hicho kutawala, kusimamia, na kudumisha kuwepo kwa vitu vyote. Ukitimiza ufahamu kama huo, utakubali kwa kweli kwamba Mungu ni Mungu wako. Ukifikia kiwango hiki, umemkubali Mungu kwa kweli na kumruhusu awe Mungu wako na Bwana wako. Ukiwa na ufahamu kama huo na maisha yako yakifikia kiwango kama hicho, Mungu hatakujaribu na kukuhukumu tena, wala Hatakuhurutisha ufanye mambo, kwa sababu unamfahamu Mungu, unajua moyo Wake, na umemkubali Mungu kwa kweli ndani ya

moyo wako. Hii ni sababu muhimu ya kuwasilisha mada hizi kuhusu utawala na usimamizi wa Mungu juu ya vitu vyote. Ni kuwapa watu maarifa na ufahamu zaidi; sio tu kukufanya ukubali, lakini kukupa maarifa zaidi na ufahamu wa utendaji wa matendo ya Mungu.

Chakula na Kinywaji cha Kila Siku Ambavyo Mungu Anawatayarishia Wanadamu

Tulikuwa tumezungumza sasa hivi kuhusu sehemu ya mazingira ya jumla, yaani, hali zilizo muhimu kwa kuendelea kuishi kwa wanadamu ambazo Mungu aliwatayarishia wanadamu tangu Alipoumba ulimwengu. Tumezungumza sasa hivi kuhusu vitu vitano, na vitu hivi vitano ndivyo mazingira ya jumla. Tunachoenda kuzungumzia baada ya hapo kinahusiana kwa karibu na kila maisha ya wanadamu katika mwili. Ni hali muhimu inayolingana zaidi na inayokubaliana zaidi na maisha ya mtu katika mwili. Kitu hiki ni chakula. Mungu alimuumba mwanadamu na akamweka ndani ya mazingira ya kuishi yanayofaa. Baadaye, mwanadamu alihitaji chakula na maji. Mwanadamu alikuwa na hitaji hilo, hivyo Mungu alimtengenezea mwanadamu matayarisho hayo. Kwa hiyo, kila hatua ya kazi ya Mungu na kila kitu Anachofanya sio maneno matupu tu, lakini vinafanyika kwa kweli. Je, chakula ni kitu ambacho watu hawawezi kukosa kuwa nacho katika maisha yao? Chakula ni muhimu zaidi kuliko hewa? Vyote ni muhimu kwa njia sawa. Vyote ni hali na vitu muhimu kwa kuendelea kuishi kwa wanadamu na kuhifadhi mwendelezo wa maisha ya binadamu. Hewa ni muhimu zaidi au maji ni muhimu zaidi? Halijoto ni muhimu zaidi au chakula ni muhimu zaidi? Vyote ni muhimu. Watu hawawezi kuchagua kwa sababu hawawezi kuishi bila chochote kati ya hivyo vyote. Hili ni tatizo halisi, si kitu unachoweza kuchagua. Hujui, lakini Mungu anajua. Unapokiona chakula, utahisi, “Siwezi kuishi bila chakula!” Lakini baada tu ya wewe kumbwa, je, ulijua kwamba ulihitaji chakula? Hungejua, lakini Mungu anajua. Ni wakati tu unapokuwa na njaa na kuona kuna matunda juu ya miti na nafaka juu ya ardhi ili uweze kula ndipo unatambua unahitaji chakula. Wakati unahisi kiu, unaona chemchemi ya maji mbele yako, na ni wakati tu unapokunywa maji ndipo unagundua unayahitaji. Maji yalitayarishwa na Mungu kwa ajili ya mwanadamu. Kuhusu chakula, haijalishi ikiwa wewe hula milo mitatu kwa siku, milo miwili kwa siku, au hata zaidi ya hiyo; kwa ufupi, chakula ni kitu ambacho wanadamu hawawezi kukosa kuwa nacho katika maisha yao ya kila siku. Ni mojawapo ya vitu muhimu vya kudumisha kuendelea kuishi kwa kawaida kwa mwili wa binadamu. Hivyo chakula hasa hutoka wapi? Kwanza, kinatoka ndani ya udongo. Udongo ulitayarishwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu. Udongo unafaa kwa kuendelea kuishi kwa mimea mbalimbali, sio tu kwa ajili ya miti au nyasi. Mungu aliwatayarishia wanadamu mbegu za kila aina ya nafaka na vyakula mbalimbali, na Akawapa wanadamu udongo na ardhi vinavyofaa ili wapande, na wakiwa na vitu hivi, wanadamu hupata chakula. Kuna aina gani za chakula? Mnapaswa kulijua hili vizuri, sivyo? Kwanza, kuna aina

mbalimbali za nafaka. Ni nini kinahusishwa katika nafaka. Ngano, mtama wa mkia wa mbweha, mtama wa proso, mchele..., inayokuwa na maganda. Mazao ya nafaka pia yametenganishwa katika aina nyingi mbalimbali. Kuna aina nyingi za mazao ya nafaka kutoka kusini mpaka kaskazini, kama vile shayiri, ngano, oti, na nafaka inayofanana na ngano. Aina mbalimbali zinafaa kukuzwa katika maeneo mbalimbali. Pia kuna aina mbalimbali za mchele. Kusini ina aina zake za mchele, iliyo ndefu zaidi na inawafaa watu kutoka kusini kwa sababu si ya kunata sana. Kwa vile hali ya nchi ni joto zaidi kusini, wanahitajika kula aina mbalimbali kama vile mchele wa indica. Hautakiwi kunata sana la sivyo hawataweza kula na watapoteza hamu yao ya kula. Mchele unaoliwa na watu wa kaskazini ni wa kunata zaidi. Kwa vile kaskazini huwa na baridi zaidi kila mara, wanahitajika kula mchele wa kunata zaidi. Kuongezea, kuna aina mbalimbali za maharagwe. Haya yanakuzwa juu ya ardhi. Pia kuna vile vinavyokuzwa chini ya ardhi, kama viazi, viazi vitamu, jimbi, na vinginevyo. Viazi huota kaskazini. Sifa ya viazi vya kaskazini ni nzuri sana. Watu wakikosa nafaka za kula, viazi vinaweza kuwa chakula kikuu cha mlo wao ili waweze kudumisha milo mitatu kwa siku. Viazi pia vinaweza kuwa ugavi wa chakula. Viazi vitamu si vizuri kama viazi kulingana na sifa, lakini bado vinaweza kutumiwa na watu kama chakula cha kudumisha milo yao mitatu kwa siku. Ikiwa nafaka hazipatikani, watu wanaweza kutumia viazi vitamu kujaza matumbo yao. Jimbi, ambalo mara nyingi huliwa na watu wa kusini, inaweza kutumiwa kwa njia hiyo, na pia inaweza kuwa chakula kikuu. Hizi ni aina mbalimbali za nafaka, muhimu kwa chakula cha watu cha kila siku. Watu hutumia nafaka mbalimbali kutengeneza nudo, mkate mdogo wa mviringo uliopikwa kwa mvuke, mchele, na nudo za mchele. Mungu ametoa aina hizi mbalimbali za nafaka kwa wanadamu kwa wingi. Kwa nini kuna aina nyingi sana? Makusudi ya Mungu yanaweza kupatikana humo: Kwa upande mmoja, ni kwa ajili ya kufaa aina mbalimbali za udongo na hali ya nchi kaskazini, kusini, mashariki, na magharibi; kwa upande mwingine, vijenzi na kadiri mbalimbali vya nafaka hizi vinakubaliana na vijenzi na kadiri mbalimbali vya mwili wa mwanadamu. Watu wanaweza tu kudumisha virutubishi na vijenzi mbalimbali vinavyohitajika kwa miili yao kwa kula nafaka hizi. Ingawa chakula cha kaskazini na chakula cha kusini ni tofauti, vina mifanano mingi kuliko tofauti. Vyakula hivi vyote vinaweza kuridhisha mahitaji ya kawaida ya mwili wa mwanadamu na vinaweza kudumisha kuendelea kuishi kwa kawaida kwa mwili wa mwanadamu. Hivyo, sababu ya aina zinazozalishwa katika maeneo mbalimbali kuwa nyingi mno ni kwamba mwili wa mwanadamu unahitaji kinachotolewa na vyakula hivyo. Wanahitaji kinachotolewa na vyakula mbalimbali vinavyokuzwa kutoka kwa udongo ili kudumisha kuendelea kuishi kwa kawaida kwa mwili wa mwanadamu na kutimiza maisha ya kawaida ya mwanadamu. Kwa ufupi, Mungu aliwafikiria sana wanadamu. Vyakula mbalimbali ambavyo Mungu aliwapa watu si vya kuchosha—ni vyenye maarifa mengi mno. Ikiwa watu wanataka kula nafaka wanaweza kula nafaka. Watu wengine hawapendi kula nudo, wanataka kula wali, na kisha wanaweza kula wali.

Kuna aina nyingi za mchele—mchele mrefu, mchele mfupi, na yote inaweza kuridhisha ladha walizo nazo watu. Kwa hiyo, watu wakila nafaka hizi—bora tu si wa kuchaguachagua kuhusu vyakula vyao—hawatakosa lishe na wanahakikishiwa kuishi kwa afya nzuri mpaka umri wa uzeeni. Hilo lilikuwa wazo la asili ambalo Mungu alikuwa nalo akilini Alipowapa wanadamu chakula. Mwili wa mwanadamu hauwezi kuishi bila vitu hivi—je, hiyo si kweli? Wanadamu hawawezi kutatua matatizo haya halisi, lakini Mungu alikuwa tayari ametayarisha na kulifikiria kabisa. Mungu alikuwa amewatayarishia wanadamu vitu zamani sana.

Mungu amempa mwanadamu zaidi ya vitu hivi tu—pia kuna mboga. Unapokula mchele, ikiwa mchele ndio kila kitu unachokula, huenda ukakosa lishe. Ikiwa kisha utakaanga kwa mafuta kidogo vyakula kadhaa kiasi kidogokidogo au uchanganye kachumbari ya kula na mlo huo, basi vitamini katika mboga hizo na kiasi kidogo cha vitu vya msingi au lishe zingine vitaweza kupeana mahitaji ya mwili wa mwanadamu kwa njia ya kawaida sana. Wakati watu hawali vyakula vikuu wanaweza pia kula matunda, sivyo? Wakati mwingine, watu wanapohitaji uowevu au lishe zingine au ladha tofauti, pia kuna mboga na matunda ya kuwapa vitu hivyo. Kwa vile udongo na hali ya nchi ya kaskazini, kusini, mashariki na magharibi ni tofauti, pia kuna aina mbalimbali za mboga na matunda. Kwa vile hali ya nchi ya kusini ni joto sana, matunda mengi na mboga ni vya aina ya kufanywa baridi vinavyoweza kusawazisha baridi na joto ndani ya miili ya watu wanapokula vitu hivyo. Kwa upande mwingine, kuna aina chache ya mboga na matunda kaskazini, lakini hata hivyo vinatosha kwa watu wa kaskazini kufurahia. Kwa hali yoyote, kwa sababu ya ustawi wa kijamii katika miaka ya hivi karibuni, kwa sababu ya kile kinachoitwa maendeleo ya kijamii, na vilevile maendeleo katika usafiri na mawasiliano vinavyounganisha kaskazini na kusini na mashariki na magharibi, watu walio kaskazini wanaweza pia kula baadhi ya matunda ya kusini na mboga, au bidhaa za mikoa kutoka kusini, hata katika mwaka mzima. Kwa njia hiyo, hata kama watu wanaweza kuridhisha hamu yao ya chakula na matamania ya vitu vya mwili, miili yao bila kujua inapatwa na viwango mbalimbali vya madhara. Hii ni kwa sababu miongoni mwa vyakula ambavyo Mungu aliwatayarishia wanadamu, kuna vyakula na matunda na mboga vinavyofaa watu walio kusini, na vilevile vyakula na matunda na mboga vinavyofaa watu walio kaskazini. Yaani, ikiwa ulizaliwa kusini, kula vitu kutoka kusini kunakufaa wewe sana. Mungu alitayarisha vyakula hivi na matunda na mboga kwa sababu kusini ina hali ya nchi mahsusi. Kaskazini ina vyakula vinavyohitajika kwa miili ya watu walio kaskazini. Lakini kwa vile watu wana hamu ya chakula ya ulafi, wamefagiliwa bila kujua katika mkondo wa maendeleo ya kijamii, na kuwafanya kukiuka sheria hizi bila kujua. Ingawa watu wanahisi kwamba maisha yao sasa ni bora zaidi, maendeleo ya kijamii kama hayo huleta madhara ya kufichika kwa miili ya watu wengi zaidi. Hiki si kile ambacho Mungu anataka kuona na vile vile si kile ambacho Mungu alikusudia alipompatia

mwanadamu vyakula hivi, matunda na mboga. Wanadamu wenyewe wamesababisha hali ya sasa kwa kukiuka sheria ambazo Mungu aliweka.

Kuongezea, kile ambacho Mungu aliwapa wanadamu ni cha fahari na kingi, kila sehemu ikiwa na vitu maalum vya mahali maalum. Kwa mfano, sehemu nyingine zina utajiri wa tende nyekundu (zinazojulikana kwa kawaida kama jujubes), ilhali zingine zina utajiri wa jozi, na zingine zina utajiri kwa karanga, au aina zingine za njugu. Vitu hivi yakinifu vyote vinampa lishe inayohitajika na mwili wa mwanadamu. Lakini Mungu huwapa wanadamu vitu kulingana na misimu na wakati, na pia anawapa kiasi sahihi kwa wakati sahihi. Wanadamu hutamani kujifurahisha kwa kimwili na ni walafi, hiyo inafanya kuwa rahisi kukiuka na kuharibu sheria za kawaida za ukuaji wa mwanadamu tangu Alipowaumba wanadamu. Kama mfano, hebu tutazame matunda ya cheri, ambazo kila mtu anapaswa kuzijua, sivyo? Hizo huiva karibu Juni. Kwa kawaida, hizo huisha kabla ya Agosti. Cheri huwa mbichi kwa miezi miwili pekee, lakini kupitia mbinu za kisayansi watu sasa wanaweza kurefusha muda huo mpaka miezi 12, hata mpaka msimu wa cheri wa mwaka unaofuata. Hiyo inamaanisha cheri zipo kwa mwaka mzima. Je, jambo hili ni la kawaida? (La.) Basi msimu bora zaidi wa kula cheri ni upi? Ni kipindi cha kuanzia Juni mpaka Agosti. Zaidi ya kikomo hiki, haijalishi utaziweka mbichi vipi, hazitakuwa na ladha sawa, wala sio kile ambacho mwili wa mwanadamu unahitaji. Mara tu tarehe ya kuisha kutumika inapopita, haijalishi ni vitu vipi vya kemikali unatumia, hutaweza kuzifanya ziwe kama zinavyokuwa wakati zinakuzwa kwa kawaida. Zaidi, madhara ambayo kemikali huleta kwa wanadamu ni kitu ambacho hakuna anayeweza kufanya chochote kuyaondoa au kuyabadilisha. Basi, ni nini ambacho soko la uchumi la wakati huu linawaletea watu? Maisha ya watu yanaonekana kuwa mazuri zaidi, usafiri katika pande zote umekuwa wa kufikika kwa urahisi sana, na watu wanaweza kula aina zote za matunda katika msimu wowote kati ya misimu minne ya mwaka. Watu wa kaskazini mara kwa mara huweza kula ndizi na chakula chochote, vitu maalum vya mahali maalum au matunda kutoka kusini. Lakini haya si maisha ambayo Mungu anataka kuwapa wanadamu. Soko hili la uchumi huleta manufaa fulani kwa maisha ya wanadamu lakini pia linaweza kuleta madhara. Kwa sababu ya wingi wa vyakula sokoni, watu wengi hula chochote, wao hula bika kufikiria. Jambo hili hukiuka sheria za asili na lina madhara kwa afya yao. Hivyo, soko la uchumi haliwezi kuletea watu furaha ya kweli. Jioneenini wenyewe. Zabibu haziuzwi sokoni katika misimu yote mine? Kwa kweli, zabibu huwa mbichi tu kwa muda wa kipindi kifupi sana baada ya kuchumwa. Ukiziweka mpaka Juni inayofuata, bado zinaweza kuitwa zabibu? Je, unaweza kuziita takataka? Hazitakosa tu vijenzi vya asili vya zabibu, lakini pia zina kemikali zaidi juu yake. Baada ya mwaka mmoja, hazijapoteza tu ubichi wake, lakini pia lishe zake zimepotea kitambo. Watu wanapokula zabibu, wanahisi: “Ninafurahi sana! Je, tungeweza kula zabibu wakati wa msimu huu miaka 30 iliyopita? Hungeweza kuzila

hata kama ungetaka. Maisha ni mazuri jinsi gani wakati huu!” Je, hii ni furaha kweli? Ukipenda, unaweza kwenda kusoma juu ya zabibu zilizohifadhiwa kwa kemikali na uone hasa vijenzi vyake ni vipi na iwapo vijenzi hivi vinaweza kuleta manufaa yoyote kwa wanadamu. Katika Enzi ya Sheria. Waisraeli walipokuwa njiani baada ya kuondoka Misri, Mungu aliwapa kware na mana. Je, Mungu aliwaruhusu watu kuvihifadhi? Wengine wao hawakufikiria mambo ya wakati ujao na waliogopa kwamba hakungekuwa na zaidi siku iliyofuata, hivyo walihifadhi nyingine iwapo wangehitaji baadaye. Kisha nini kilifanyika? Kufikia siku iliyofuata ilikuwa imeoza. Mungu hakuwaruhusu kuweka nyingine kama akiba kwa sababu Mungu alikuwa amefanya matayarisho fulani, yaliyohakikisha hawangekufa kwa njaa. Wanadamu hawana hakika hiyo, wala hawana imani ya kweli kwa Mungu. Kila mara wanaweka nyengine kando kwa ajili ya baadaye na hawawezi kamwe kuona utunzi wote na mawazo yaliyo ndani ya kile ambacho Mungu amewatayarishia wanadamu. Kila mara hawawezi kuhisi hasa, kila mara wanakosa kumwamini Mungu, kila mara wanafikiria: “Matendo ya Mungu si ya kutegemewa! Nani anajua iwapo Mungu atawapa wanadamu au ni lini Atawapa! Ikiwa nina njaa sana na Mungu hanipi, basi si nitakufa njaa? Si nitakosa lishe?” Ona jinsi hakika ya mwanadamu ni ndogo sana!

Nafaka, matunda na mboga, na kila aina ya njugu vyote ni vyakula vya wala mboga. Hata kama ni vyakula vya wala mboga, vina lishe za kutosha kuridhisha mahitaji ya mwili wa mwanadamu. Kwa hali yoyote, Mungu hakusema: “Kuwapa wanadamu hiki kunatosha. Wanadamu wanaweza tu kula vitu hivi.” Mungu hakuachia hapo na badala yake aliwatayarishia wanadamu vitu vyenye ladha nzuri zaidi. Vitu hivi ni gani? Ni aina mbalimbali ya nyama na samaki wengi wenu mnaweza kuona na kula kila siku. Kuna aina nyingi sana za nyama na samaki ambazo Mungu amemtayarishia mwanadamu. Samaki wote huishi majini; umbile asili la nyama yao ni tofauti na la nyama inayokuzwa juu ya ardhi na wanaweza kuwapa wanadamu lishe mbalimbali. Sifa za samaki zinaweza kubadilisha baridi na joto ndani ya mwili wa mwanadamu, kwa hiyo ni za manufaa makubwa sana kwa wanadamu. Lakini kilicho na ladha nzuri hakitakiwi kuliwa zaidi. Bado msemu ni huo huo: Mungu huwapa wanadamu kiasi sahihi kwa wakati sahihi, ili watu waweze kufurahia kwa kawaida na vizuri vitu hivi kulingana na msimu na wakati. Ndege wa kufugwa wanahusisha nini? Kuku, kware, njiwa, n.k. Watu wengi hula pia bata na bata bukini. Ingawa Mungu alitayarisha aina hizi za nyama, Alitoa masharti fulani kwa watu Wake aliowachagua na kuweka mipaka maalum kwa chakula chao wakati wa Enzi ya Sheria. Sasa eneo hili linatojkana na kupendelea kwa mtu binafsi na ufahamu wa mtu binafsi. Aina hizi mbalimbali za nyama hupatia mwili wa mwanadamu lishe mbalimbali, zinazoweza kusheheneza protini na madini ya chuma, kusitawisha damu, kuimarisha misuli na mifupa, na kupeana nguvu zaidi. Haijalishi ni mbinu gani watu hutumia kupika na kula vitu hivyo, kwa ufupi, vitu hivi vinaweza kwa upande mmoja kuwasaidia watu kuendeleza ladha na

hamu ya chakula, na kwa upande mwingine kuridhisha matumbo yao. Kitu cha muhimu zaidi ni kwamba zinaweza kupatia mwili wa mwanadamu mahitaji yao ya lishe ya kila siku. Hizi ndizo fikira ambazo Mungu alikuwa nazo Alipowatayarishia wanadamu chakula. Kuna vyakula vya wala mboga na pia nyama—je, hiyo si ya fahari na nyingi? Lakini watu wanapaswa kuelewa kusudi la asili la Mungu lilikuwa gani Mungu alipowatayarishia wanadamu vyakula vyote. Je, ilikuwa ni kuwafanya wanadamu kutumia kupita kiasi hivi vyakula? Nini hutendeka wakati mtu hunaswa kwa kujaribu kuridhisha tamaa hizi za vitu? Je, hapati lishe ya kupita kiasi? Je, lishe ya kupita kiasi haidhuru mwili wa mwanadamu kwa njia nyingi? (Ndiyo.) Hiyo ndiyo maana Mungu hutoa kiasi sahihi kwa wakati sahihi na kuwaacha watu wafurahie vyakula mbalimbali kulingana na vipindi vya wakati na misimu. Kwa mfano, baada ya kuishi katika majira ya joto sana, watu watakusanya kiasi fulani cha joto, la kusababisha ukavu wa viini na unyevunyevu katika miili yao. Majira ya kupukutika kwa majani yakija, matunda ya aina nyingi sana yataiva, na watu watakapokula baadhi ya tunda unyevunyevu wao utaondolewa. Wakati huo huo, ng’ombe na kondoo watakuwa wamekua na kupata nguvu, ili watu wale nyama kiasi kama lishe. Baada ya kula aina mbalimbali za nyama, miili ya watu itakuwa na nguvu na joto la kuisaidia kustahimili baridi ya majira ya baridi, na kutokana na hayo wataweza kupita katika majira ya baridi kwa amani. Wakati upi wa kutayarisha vitu vipi kwa ajili ya wanadamu, na wakati upi wa kuacha vitu vipi vikue, vizae matunda na kuiva—yote haya yanadhibitiwa na kupangwa na Mungu kwa kupimwa kabisa. Hii ni mada kuhusu “jinsi Mungu alitayarisha chakula kilicho muhimu kwa maisha ya mwanadamu ya kila siku.” Mbali na aina zote za chakula, Mungu pia huwapa wanadamu vyanzo vya maji. Watu huhitaji kunywa maji kiasi baada ya kula. Je, kula matunda tu kunatosha? Watu hawataweza kustahimili kula matunda pekee, licha ya hayo, huwa hakuna matunda katika misimu mingine. Hivyo tatizo la wanadamu la maji litawezaje kutatuliwa? Kwa Mungu kutayarisha vyanzo vingi vya maji juu ya ardhi na chini ya ardhi, ikiwemo maziwa, mito, na chemchemi. Vyanzo hivi vya maji vinaweza kunywewa maji katika hali ambazo hakuna kuchafuliwa kokote, au maendeleo ya wanadamu au uharibifu. Yaani, kuhusu vyanzo vya chakula kwa maisha ya miili ya wanadamu, Mungu amefanya matayarisho sahihi sana, yasiyo na hitilafu yoyote na ya kufaa sana, ili maisha ya watu yawe ya fahari na yenye wingi na yasiyokosa chochote. Hiki ni kitu ambacho watu wanaweza kuhisi na kuona.

Kuongezea, miongoni mwa vitu vyote Mungu aliumba baadhi ya mimea, wanyama, na mitishamba mbalimbali ambayo hususan hokusudiwa kuponya majeraha ama kutibu magonjwa katika mwili wa mwanadamu. Utafanya nini, kwa mfano, ukichomeka au kuungua kiajali na maji moto? Je, unaweza kufoka kwa maji? Je, unaweza kutafuta kitambaa na kufunika mahali hapo? Huenda pakajaa usaha au kuambukizwa kwa njia hiyo. Kwa mfano, ukipata homa, upate mafua, upate majeraha kutokana na kazi ya viungo, maradhi ya tumbo kutokana na kula kitu kibaya, au

kupata magonjwa fulani kwa sababu ya mienendo ya maisha au masuala ya hisia, kama vile magonjwa ya mishipa ya damu, hali za kisaikolojia au magonjwa ya ogani zilizo ndani ya mwili—kuna mimea inayolingana ya kutibu haya yote. Kuna mimea inayoendeleza mzunguko wa damu kuondoa ukwamaji, kutuliza maumivu, kukomesha kutokwa na damu, kutia ganzi, kuwasaidia watu kupata tena ngozi ya kawaida, kuondoa ukwamaji wa damu mwilini, na kuondoa sumu mwilini. Kwa ufupi, yote inaweza kutumiwa katika maisha ya kila siku. Ni ya kufaa watu na imetayarishwa na Mungu kwa ajili ya mwili wa mwanadamu iwapo inahitajika. Baadhi ya hiyo iliruhusiwa na Mungu kugunduliwa bila uangalifu na mwanadamu, ilhali mingine iligunduliwa na watu ambao Mungu aliwachagua kufanya hivyo, ama kama matokeo ya matukio maalum Aliyoyapanga. Baada ya ugunduzi wao, wanadamu wangeipitisha kwa wengine, na halafu watu wengi wangejua kuihusu. Kwa njia hii, uumbaji wa Mungu wa mimea hii unakuwa na thamani na maana. Kwa ufupi, vitu hivi vyote vinatoka kwa Mungu na vilitayarishwa na kupandwa Alipowaambia wanadamu mazingira ya kuishi. Vitu hivi vyote ni muhimu sana. Je, fikira Zake Mungu zilifikiriwa vizuri sana kuliko za wanadamu? Unapooni yote ambayo Mungu amefanya, unaweza kuhisi upande wa Mungu wa vitendo? Mungu alifanya kazi katika siri. Kabla ya mwanadamu kuingia katika ulimwengu huu, kabla ya kukutana na wanadamu hawa, Mungu alikuwa tayari ameviumba vitu hivi vyote. Kila kitu alichofanya kilikuwa kwa ajili ya wanadamu, kwa ajili ya kuendelea kuishi kwao, na kwa ajili ya kufikiria juu ya kuwepo kwa wanadamu, ili wanadamu waweze kuishi kwa furaha katika ulimwengu huu yakinifu wa ufahari na wingi ambao Mungu aliwatayarishia, bila kuwa na wasiwasi kuhusu chakula au nguo, na bila kukosa chochote. Wanadamu wanaendelea kuzaa na kuendelea kuishi katika mazingira hayo.

Kuna chochote ambacho Mungu hufanya, bila kujali iwapo kitu hicho ni kikubwa au kidogo, kisicho na thamani au maana? Kila kitu Afanyacho kina thamani na maana. Tujadili hili kutoka kwa swali ambalo watu mara nyingi hulizungumzia. Watu wengi huuliza: Ni kipi kilitangulia, kuku au yai? (Kuku.) Je, utajibuje hili? Kuku alitangulia, hapana shaka juu ya hili! Kwa nini kuku alitangulia? Kwa nini yai halingeweza kutangulia? Kuku haanguliwi kutoka kwa yai? Baada ya siku 21, kuku huangua na huyo kuku hutaga mayai zaidi, na kuku zaidi huanguliwa kutoka kwa hayo mayai. Hivyo kuku alitangulia au yai lilitangulia? Mnajibu “kuku” kwa uhakika. Kwa nini? (Biblia inasema Mungu aliumba ndege na wanyama wa mwitu.) Hiyo ina msingi katika Biblia. Ninataka mzungumze kuhusu maarifa yenu wenyewe kuona iwapo mna maarifa ya kweli ya matendo ya Mungu. Je, mna hakika kuhusu jibu lenu au la? (Mungu aliumba kuku, halafu akampa uwezo wa kuzaa, yaani uwezo wa kuatamiza mayai) Maelezo haya yanakaribia kuwa sahihi. Kuku alikuwa wa kwanza, na kisha yai. Huo ndio utaratibu.) Kuku alitangulia. Hili ni hakika. Si fumbo la maana sana, lakini watu wa dunia

huliona kuwa la maana sana na hutumia falsafa kwa utoaji hoja. Mwishowe, bado huwa hawana hitimisho. Jambo hili ni kama wakati watu hawajui kwamba Mungu aliwaumba. Hawajui kanuni hii muhimu, wala hawana uhakika kuhusu iwapo yai au kuku anapaswa kutangulia. Hawajui ni nini kinapaswa kutangulia, hivyo kila mara wao hushindwa kupata jibu. Ni kawaida kabisa kwamba kuku alitangulia. Ikiwa yai lingetangulia kabla ya kuku, basi hiyo haingekuwa kawaida! Bila shaka kuku alitangulia. Hiki ni kitu rahisi sana. Hakiwahitaji nyinyi kuwa wenye maarifa mengi. Mungu aliumba hivi vyote. Kusudi Lake la mwanzo lilikuwa ni mwanadamu kuvifurahia. Kuku akiwepo, yai linakuja kwa kawaida. Je, hili si suluhisho rahisi? Ikiwa yai lingeumbwa kwanza, je, bado halingehitaji kuku kuliitamiza? Kuumba kuku moja kwa moja ni suluhisho rahisi zaidi. Kwa njia hii, kuku angezaa mayai na kuatamiza vifaranga walio ndani, na watu wanguweza kuwa na kuku wa kula. Jambo la kufaa kweli! Vile Mungu afanyavyo mambo ni kwa maneno machache ya wazi na sio kwa usumbufu. Yai linatoka wapi? Linatoka kwa kuku. Hakuna yai bila kuku. Alichoumba Mungu ni kiumbe chenye uhai! Wanadamu ni wa upuuzi na wa dhihaka, kila mara wanajitatanisha katika mambo haya rahisi, na mwishowe hata wanafikia kifungu kizima cha hoja za uwongo. Hayo ni ya kitoto! Uhusiano kati ya yai na kuku ni dhahiri: Kuku alitangulia. Hayo ndiyo maelezo sahihi kabisa, njia sahihi kabisa ya kulielewa, na jibu sahihi kabisa. Hii ni ya kweli.

Tumetoka kuzungumzia nini? Hapo mwanzo, tulizungumza kuhusu mazingira ya kuishi ya wanadamu na kile Mungu alifanya, alitayarisha, na kushughulikia kwa ajili ya mazingira haya, na vilevile mahusiano kati ya vitu vyote ambavyo Mungu aliwatayarishia wanadamu na jinsi Mungu alishughulikia mahusiano haya yote kuzuia vitu vyote kuleta madhara kwa wanadamu. Mungu pia alitatu athari hasi katika mazingira ya wanadamu zilizosababishwa na vitu mbalimbali vya asili ambavyo vinaletwa na mambo yote, Akaruhusu vitu vyote kuongeza hadi upeo shughuli za vitu hivyo, na Akawaletwa wanadamu mazingira ya kufaa na vitu vyote vya asili vyenye manufaa, kuwawezesha wanadamu kuwa wepesi kubadilika kwa mazingira hayo na kuendelea na mfuatano wa kuzaa na wa maisha kwa kawaida. Kilichofuata kilikuwa chakula kilichohitajika na mwili wa mwanadamu—chakula cha kila siku na kinywaji. Hii pia ni hali muhimu ya kuendelea kuishi kwa mwanadamu. Hiyo ni kusema, mwili wa mwanadamu hauwezi kuishi tu kwa kupumua, kuwa na mwangaza wa jua au upepo pekee, au halijoto za kufaa tu. Wanahitaji pia kujaza matumbo yao. Vitu hivi vya kujaza matumbo yao vyote vimetayarishwa pia na Mungu kwa ajili ya wanadamu—hiki ni chanzo cha chakula cha wanadamu. Baada ya kuona mazao haya ya fahari na mengi—vyanzo vya chakula cha wanadamu na kinywaji—unaweza kusema kwamba Mungu ni chanzo cha kupeana wanadamu na vitu vyote? Ikiwa Mungu angeumba tu miti na nyasi au hata viumbe mbalimbali vyenye uhai Alipoumba vitu vyote, ikiwa hivyo viumbe mbalimbali vyenye uhai vyote vingekuwa vya ng’ombe na kondoo

kula, au vingekuwa vya pundamilia, paa na aina nyingine mbalimbali za wanyama, kwa mfano, simba walipaswa kula vitu kama pundamilia na paa, na chui wakubwa wenye milia walipaswa kula vitu kama kondoo na nguruwe—lakini kusiwe na hata kitu kimoja cha kufaa wanadamu kula, je, hilo lingefaulu? Halingefaulu. Wanadamu hawangeweza kuendelea kuishi. Na je, wanadamu wangekula tu majani ya miti? Hilo lingefaulu? Wanadamu wangeweza kula nyasi ambayo kondoo hutayarishiwa? Huenda ikawa sawa wakijaribu kidogo tu, lakini wakiendelea kula kwa muda mrefu, matumbo ya wanadamu hayataweza kustahimili tena na hawatadumu kwa muda mrefu. Na hata kuna vitu vingine ambavyo vinaweza kuliwa na wanyama, lakini wanadamu wakivila watapata sumu. Kuna vitu vingine vyenye sumu ambavyo wanyama wanaweza kuvila bila kuathiriwa, lakini wanadamu hawawezi kufanya vivyo hivyo. Kwa maneno mengine, Mungu aliwaumba wanadamu, hivyo Mungu anajua vizuri sana kanuni na muundo wa mwili wa mwanadamu na wanachohitaji wanadamu. Mungu ana hakika kamili kuhusu sehemu na vijenzi vyake, na inachohitaji, vilevile jinsi sehemu za ndani ya mwili wa mwanadamu hufanya kazi, hufyonza, huondosha, na kuvunjavunja kemikali mwilini. Watu hawana hakika kuhusu hili na wakati mwingine hula na kujaliza bila kujua. Wao hujaliza kupita kiasi na mwisho husababisha kutolingana nguvu. Ukila na kufurahia vitu hivi alivyokutayarishia Mungu kwa kawaida, hutakuwa na shida yoyote. Hata kama wakati mwingine una hali mbaya ya moyo na una ukwamaji wa damu, haidhuru. Unahitaji tu kula aina fulani ya mmea na ukwamaji utatatuliwa. Mungu ametayarisha vitu hivi vyote. Kwa hivyo, machoni mwa Mungu, wanadamu wako juu zaidi ya kiumbe chochote kingine chenye uhai. Mungu alitayarishia kila aina ya mimea mazingira ya kuishi na Akatayarishia kila aina ya wanyama chakula na mazingira ya kuishi, lakini mahitaji ya wanadamu pekee kwa mazingira yao ya kuishi ndiyo makali zaidi na yasiyostahimili kutotunzwa. La sivyoyote, wanadamu hawangeweza kuendelea kukua na kuzaa na kuishi kwa kawaida. Mungu anajua hili vizuri zaidi moyoni Mwake. Mungu alipofanya hili, alilipa umuhimu zaidi kuliko kitu chengine chochote. Labda huwezi kuhisi umuhimu wa kitu fulani kisicho na maana unachokiona na kufurahia au kitu unachohisi ulizaliwa nacho na unaweza kufurahia, ilhali kisiri, au pengine muda mrefu uliopita, Mungu alikuwa tayari amekutayarishia hekima Yake. Mungu ameondoa na kutatua kwa kiwango kikubwa zaidi iwezekanavyo vipengele vyote hasi visivyofaa kwa wanadamu na vinavyoweza kudhuru mwili wa mwanadamu. Nini ambacho hiki kinaweka wazi? Je, kinahakikisha mtazamo wa Mungu kwa wanadamu Alipowaumba wakati huu? Mtazamo huo ulikuwa upi? Mtazamo wa Mungu ulikuwa wa msimamo na maana kubwa, na Hakustahimili kuingilia kati kwa vipengele au hali au nguvu zozote za adui isipokuwa Mungu. Kutokana na hili, unaweza kuona mtazamo wa Mungu alipoumba wanadamu na katika usimamizi Wake wa wanadamu wakati huu. Mtazamo wa Mungu ni upi? Kupitia kwa mazingira ya kuishi na kuendelea kuishi ambayo wanadamu wanafurahia pamoja na chakula chao cha kila siku na kinywaji na mahitaji ya kila siku, tunaweza

kuona mtazamo wa Mungu wa wajibu kwao wanadamu ambao Anao tangu Awaumbe, na vilevile uamuzi wa Mungu wa kuwaokoa wanadamu wakati huu. Je, tunaweza kuona uhalisi wa Mungu kupitia kwa haya yote? Tunaweza kuona ustaajibishaji wa Mungu? Tunaweza kuona kutoweza kueleweka kwa Mungu? Tunaweza kuona kudura ya Mungu? Mungu anatumia tu njia Zake za uweza na hekima kuwapa wanadamu wote, na vilevile kuvipa vitu vyote. Licha ya hayo, baada ya Mimi kusema mengi sana, mnaweza kusema kwamba Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote? (Ndiyo.) Hili ni hakika. Je, mna shaka yoyote? (La.) Upeanaji wa Mungu wa vitu vyote ni wa kutosha kuonyesha kwamba Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote, kwa sababu Yeye ni chanzo cha ruzuku ambao umewezesha vitu vyote kuwepo, kuishi, kuzaa, na kuendelea, na hakuna chanzo kingine ila Mungu Mwenyewe. Mungu huruzuku mahitaji yote ya vitu vyote na mahitaji yote ya wanadamu, bila kujali iwapo ni mazingira ya msingi kabisa ya watu kuishi, wanachohitaji watu kila siku, au upeanaji wa ukweli kwa roho za watu. Kutokana na mitazamo yote, inapofikia utambulisho wa Mungu na hadhi Yake kwa wanadamu, ni Mungu Mwenyewe pekee ndiye chanzo cha uhai kwa vitu vyote. Hili ni sahihi? (Ndiyo.) Yaani, Mungu ni Mtawala, Bwana, na Mpaji wa dunia hii yakinifu ambayo watu wanaweza kuona kwa macho yao na kuhisi. Kwa wanadamu, je, huu si utambulisho wa Mungu? Hii ni kweli kabisa. Hivyo unapoondege wakiruka angani, unapaswa kujua kwamba Mungu aliumba vitu vinavyoweza kuruka. Lakini kuna viumbe vyenye uhai vinavyoogelea majini, navyo pia huendelea kuishi kwa njia mbalimbali. Miti na mimea inayoishi ndani ya udongo huchipuka katika majira ya kuchipuka na huzaa matunda na kupoteza majani katika majira ya kupukutika kwa majani, na ifikapo wakati wa majira ya baridi majani yote huwa yameanguka na kupitia katika majira ya baridi. Hiyo ni njia yao ya kuendelea kuishi. Mungu aliumba vitu vyote, na kila kimojawapo huishi kupitia taratibu mbalimbali na njia mbalimbali na hutumia mbinu mbalimbali kuonyesha nguvu zake na taratibu ya maisha. Haijalishi ni mbinu gani, yote iko chini ya utawala wa Mungu. Ni nini kusudi la Mungu la kutawala taratibu zote mbalimbali za maisha na viumbe vyenye uhai? Je, ni kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa wanadamu? (Ndiyo.) Anadhibiti sheria zote za maisha kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa wanadamu. Hii inaonyesha hasa vile kuendelea kuishi kwa wanadamu ni muhimu kwa Mungu.

Wanadamu kuweza kuendelea kuishi na kuzaa kwa kawaida ni jambo la muhimu zaidi kwa Mungu. Kwa hiyo, Mungu daima huwapa wanadamu na vitu vyote. Anapeana vitu vyote kwa njia mbalimbali, na chini ya hali za kudumisha kuendelea kuishi kwa vitu vyote, Anawawezesha wanadamu kuendelea kusonga mbele ili Aweze kudumisha kuwepo kwa kawaida kwa wanadamu. Hivi ndivyo vipengele viwili tunavyowasiliana leo. Vipengele hivi ni vipi? (Kutokana na mtazamo mkubwa, Mungu aliwaambia wanadamu mazingira ya kuishi. Hicho ni kipengele cha kwanza. Pia, Mungu alitayarisha hivi vitu yakinifu ambavyo wanadamu wanahitaji

na wanaweza kuona na kugusa.) Tumewasilisha mada yetu kuu kupitia vipengele hivi viwili. Mada yetu kuu ni gani? (Mungu Ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote.) Mnapaswa sasa kuwa na ufahamu fulani wa mbona Niliwasilisha maudhui haya chini ya mada hii. Je, kumekuwa na majadiliano yoyote yasiyohusiana na mada kuu? Hakuna, sivyo? Labda baada ya kusikia mambo haya, wengine wenu hupata ufahamu fulani na kuhisi kwamba maneno haya ni muhimu sana, lakini wengine huenda wakapata tu ufahamu kidogo wa kawaida na kuhisi kwamba maneno haya hayana maana. Haijalishi vile nyinyi mnaelewa hili wakati huu, mnapoendelea kupitia matukio itafika siku ambayo ufahamu wenu utafikia kiwango fulani, yaani, wakati maarifa yenu ya matendo ya Mungu na Mungu Mwenyewe yatafikia kiwango fulani, mtatumia maneno yenu wenyewe ya kiutendaji kuwasilisha ushuhuda wa maana na wa kweli kuhusu matendo ya Mungu.

Ninafikiri ufahamu wenu sasa bado ni sahili na wa kawaida, lakini mnaweza angaa, baada ya kunisikiliza Nikiwasilisha vipengele hivi viwili, kutambua ni mbinu zipi Mungu hutumia kuwapa wanadamu au ni vitu vipi Mungu huwapa wanadamu? Je, mna wazo la msingi na vilevile ufahamu wa msingi? (Ndiyo.) Lakini vipengele hivi viwili Nilivyowasilisha vinahusiana na Biblia? (La.) Vinahusiana na hukumu na kuadibu kwa Mungu katika Enzi ya Ufalme? (La.) Basi kwa nini Niliwasilisha vipengele hivi? Je, ni kwa sababu watu ni lazima wavielewe ili kumjua Mungu? (Ndiyo.) Ni muhimu sana kuvijua na pia ni muhimu sana kuvielewa. Usizuiwe tu kwa Biblia, na usizuiwe tu kwa Mungu kuhukumu na kuadibu wanadamu ili kuelewa kila kitu kuhusu Mungu. Ni nini kusudi la Mimi kusema hili? Ni ili kuwafanya watu wajue kwamba Mungu si Mungu wa watu Wake wateule pekee. Wewe sasa unamfuata Mungu, na Yeye ni Mungu wako, lakini kwa wale walio nje ya watu wanaomfuata Mungu, je, Mungu ni Mungu wao? Je, Mungu ni Mungu wa watu wote walio nje ya wale wanaomfuata Yeye? Mungu ni Mungu wa vitu vyote? (Ndiyo.) Basi Mungu hutenda kazi Yake na kutekeleza matendo Yake kwa wale tu wanaomfuata Yeye? (La.) Mawanda ya kazi Yake na matendo Yake ni yapi? Kwa kiwango kidogo zaidi, mawanada ya kazi Yake na matendo Yake yanajumuisha wanadamu wote na vitu vyote vya uumbaji. Kwa kiwango cha juu inajumuisha ulimwengu wote ambao watu hawawezi kuuona. Hivyo tunaweza kusema kwamba Mungu hufanya kazi Yake na kutekeleza matendo Yake miongoni mwa wanadamu wote. Hili ni la kutosha kuwafanya watu wajue yote kuhusu Mungu Mwenyewe. Ikiwa unataka kumjua Mungu na upate kweli kumjua na kumfahamu Yeye, basi usizuiwe tu katika hatua tatu za kazi ya Mungu, na usizuiwe tu katika hadithi za kazi ambayo Mungu alitekeleza wakati mmoja. Ukijaribu kumjua hivyo, basi unajaribu kumzuilia Mungu kwa mipaka fulani. Wewe unamwona Mungu kitu kidogo Ni jinsi gani kufanya hivyo kungeathiri watu? Hungeweza kujua maajabu na mamlaka ya juu kabisa ya Mungu, na hungeweza kamwe kujua nguvu za Mungu na kudura na eneo la mamlaka Yake.

Ufahamu kama huo ungeathiri uwezo wako wa kukubali ukweli kwamba Mungu ni Mtawala wa vitu vyote, na vilevile maarifa yako ya utambulisho wa kweli na hadhi ya Mungu. Kwa maneno mengine, iwapo ufahamu wako wa Mungu umewekewa mipaka katika eneo, unachoweza kupokea pia kimewekewa mipaka. Ndiyo maana ni lazima upanue eneo na kufungua upeo wa macho yako. Iwe ni eneo la kazi ya Mungu, usimamizi wa Mungu, na utawala wa Mungu, au vitu vyote vinavyotawaliwa na kusimamiwa na Mungu, unapaswa kujua yote na kupata kujua matendo ya Mungu yaliyo ndani. Kupitia njia hii ya ufahamu, utahisi bila kujua kwamba Mungu anatawala, anasimamia na kupeana vitu vyote miongoni mwao. Wakati huo huo, utahisi kweli kwamba wewe ni sehemu ya vitu vyote, na kiungo cha vitu vyote. Mungu anapovipa vitu vyote, wewe pia unakubali utawala na upeanaji wa Mungu. Huu ni ukweli usioweza kupingwa na yeyote. Vitu vyote viko chini ya mamlaka ya sheria zao, ambazo ziko chini ya utawala wa Mungu, na vitu vyote vina sheria zao za kuendelea kuishi, ambazo pia ziko chini ya utawala wa Mungu, huku majaliwa ya wanadamu na wanachohitaji pia vikihusiana kwa karibu na utawala wa Mungu na upeanaji Wake. Ndiyo maana, chini ya utawala wa Mungu na uongozi, wanadamu na vitu vyote vinahusiana, vinategemeana, na vinafumana. Hili ni kusudi na thamani ya uumbaji wa Mungu wa vitu vyote. Unaelewa hili sasa, sivyo? Basi baada ya hayo, acha tuhitimishe ushirika wa leo Kwaheri! (Shukrani kwa Mungu!)

Februari 2, 2014

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee IX

Mungu ni Chanzo cha Uzima kwa Vitu Vyote (III)

Kwa kipindi hiki chote, tumezungumza juu ya mambo mengi yanayohusiana na kumjua Mungu na hivi karibuni tulizungumza kuhusu kitu fulani muhimu sana juu ya hii. Ni mada gani? (Mungu ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote.) Inaonekana yale mambo na mada niliyoyazungumzia yaliwachia kila mtu wazo dhahiri. Wakati uliopita tulizungumza juu ya vipengele vichache vya mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo Mungu aliyatengeneza kwa ajili ya binadamu, vilevile Mungu kuandaa kila aina ya riziki ya lazima kwa ajili ya watu katika maisha yao. Kwa kweli, kile ambacho Mungu anafanya si tu kuandaa mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa watu wala si tu kuandaa riziki yao ya kila siku, bali ni kuandaa vipengele mbalimbali vya kazi kubwa ya ajabu na ya lazima kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa watu na kwa ajili ya maisha ya binadamu. Haya yote ni matendo ya Mungu. Matendo haya yanayofanywa na Mungu hayakomei tu kwenye maandalizi Yake ya mazingira kwa ajili ya watu kuendelea kuishi na riziki zao za kila siku—yana mawanda mapana zaidi kuliko hayo. Licha ya aina mbili hizi za kazi, pia Anaandaa mazingira mengi na hali kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo ni lazima kwa ajili ya maisha ya mwanadamu. Hii ndiyo mada ambayo tutajadili leo. Pia

inahusiana na matendo ya Mungu; vinginevyo, kuizungumzia hapa isingekuwa na maana. Ikiwa watu wanataka kumjua Mungu lakini wana maana ya moja kwa moja ya “Mungu,” ya neno hilo, au ya vipengele vyote vya kile Mungu anacho na alichio, huo sio uelewa wa kweli. Sasa, njia kwa ajili ya maarifa ya Mungu ni ipi? Ni kumjua Yeye, kujua kila kipengele Chake kupitia matendo Yake. Kwa hiyo, kinachofuata tunapaswa kushiriki kuhusu matendo ya Mungu pale alipoumba vitu vyote.

Tangu Mungu alipoviumba, kulingana na sheria ambazo Aliziamua, vitu vyote vimekuwa vikitenda kazi na vimekuwa vikiendelea kukua kwa kawaida. Chini ya uangalizi Wake, chini ya kanuni Yake, vitu vyote vimekuwa vikiendelea kwa kawaida sambamba na kuendelea kuishi kwa binadamu. Hakuna kitu hata kimoja kinaweza kubadilisha sheria hizi, na hakuna hata kitu kimoja kinachoweza kuziharibu sheria hizi. Ni kwa sababu ya kanuni ya Mungu ndipo viumbe vyote vinaweza kuongezeka, na kwa sababu ya kanuni na usimamizi Wake ndipo vitu vyote vinaweza kuendelea kuishi. Hii ni kusema kwamba chini ya kanuni ya Mungu, viumbe vyote vinakuwepo, vinastawi, vinatoweka, na kuzaliwa upya kwa namna ya mpangilio. Msimu wa machipuo unapowadia, mvua ya manyunyu huleta hisia hiyo ya machipuo na kuipatia nchi unyevunyevu. Ardhi huanza kuyeyuka, na majani huota na kujipenyeza juu ya udongo na kuanza kuchipuka, ilihali miti kwa utaratibu hubadilika kuwa ya kijani. Viumbe hai hivi vyote vinaleta uzima mpya katika dunia. Hii ndiyo picha ya viumbe vyote kuwepo na kustawi. Wanyama wa kila aina pia hutoka matunduni mwao ili kupata uvuguvugu wa msimu wa machipuo na kuanza mwaka mpya. Viumbe vyote vinaota jua kwenye joto wakati wa kiangazi na kufurahia uvuguvugu unaoletwa na msimu huu. Vinakua haraka; miti, nyasi, na aina zote za mimea inakua haraka sana, kisha inachanua na kuzaa matunda. Viumbe vyote vinakuwa vimetingwa sana wakati wa kiangazi, binadamu wakiwemo. Katika msimu wa majani kupukutika, mvua inaleta utulivu wa msimu wa majani kupukutika, na aina zote za viumbe hai vinaanza kuhisi majilio ya msimu wa kiangazi. Viumbe vyote vinazaa matunda, na binadamu wanaanza kuvuna matunda haya ya aina mbalimbali ili kuwa na chakula kwa ajili ya msimu wa baridi. Katika msimu wa baridi viumbe vyote taratibu vinaanza kupumzika katika ubaridi, kuwa kimya, na watu pia wanachukua pumziko wakati wa msimu huu. Mabadiliko haya kutoka msimu wa machipuo kwenda msimu wa kiangazi kwenda msimu wa mapukutiko na kwenda msimu wa baridi—mabadiliko haya yote yanatokea kulingana na sheria zilizoanzishwa na Mungu. Anaongoza vitu vyote na wanadamu kwa kutumia sheria hizi na amebuni maisha yenye utajiri na ya kupendeza kwa ajili ya mwanadamu, akiandaa mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo yana halijoto tofautitofauti na misimu tofautitofauti. Chini ya mazingira haya yaliyopangiliwa kwa ajili ya kuendelea kuishi, binadamu wanaweza kuendelea kuishi na kuongezeka kwa namna ya mpangilio. Wanadamu hawawezi kuzibadilisha sheria hizi, na hakuna mtu hata mmoja au

kiumbe ambacho kinaweza kuzivunja. Ingawa mabadiliko yasiyohesabika yametokea—bahari zimekuwa mbuga, ilhali mbuga zimekuwa bahari—sheria hizi zinaendelea kuwepo. Sheria hizi zipo kwa sababu Mungu yupo, na kwa sababu ya sheria na usimamizi Wake. Kwa aina hii ya mpangilio, mazingira makubwa, maisha ya watu yanaendelea ndani ya sheria na kanuni hizi. Sheria hizi ziliendeleza kizazi baada ya kizazi cha watu na kizazi baada ya kizazi cha watu wameendelea kuishi ndani ya sheria hizi. Watu wamefurahia mazingira haya ya mpangilio kwa ajili ya kuendelea kuishi vilevile vyote miongoni mwa vingi vilivyoumbwa na Mungu kwa ajili ya kizazi baada ya kizazi cha binadamu. Ingawa watu wanahisi kwamba aina hii ya sheria ni za kiasili, ingawa wanazipuuza kabisa sheria hizo, na ingawa hawawezi kuhisi kuwa Mungu ndiye anaweka utaratibu wa sheria hizi, kwamba Mungu anatawala sheria hizi, haijalishi, Mungu siku zote anajihusisha katika kazi hii isiyobadilika. Kusudi lake katika kazi hii isiyobadilika ni kwa ajili ya binadamu kuendelea kuishi, na ili binadamu waweze kuendelea.

Mungu Huweka Mipaka kwa ajili ya Vitu Vyote ili Kuwalea Binadamu Wote

Leo Mimi nitazungumzia mada ya jinsi ambavyo hizi kanuni ambazo Mungu amezileta kwa vitu vyote hulea wanadamu wote. Hii ni mada kubwa, kwa hiyo tunaweza kuigawanya katika sehemu kadhaa na kuzijadili moja baada ya nyingine ili ziweze kufafanuliwa vizuri kwenu. Kwa njia hii itakuwa rahisi kwenu kupata maana na taratibu mnaweza kuielewa.

Kwanza, Mungu alipoviumba vitu vyote, Aliweka mipaka kwa ajili ya milima, tambarare, majangwa, vilima, mito, na maziwa. Duniani kuna milima, tambarare, majangwa, vilima, vilevile vyanzo mbalimbali vya maji. Je, hayo si mandhari tofautitofauti? Mungu aliweka mipaka kati ya mandhari haya yote tofautitofauti. Tunapozungumza juu ya kuweka mipaka, ina maana kwamba milima ina mipaka yake, tambarare zina mipaka yake, majangwa yana mawanda fulani, na vilima vina eneo mahususi. Pia kuna kiwango mahususi cha vyanzo vya maji kama vile mito na maziwa. Yaani, Mungu alipoumba vitu vyote aligawanya kila kitu vizuri kabisa. Mungu ameshajua nusu kipenyo cha mlima ni kilometa ngapi, mawanda yake ni mapana kiasi gani. Mungu ameshajua nusu kipenyo cha tambarare ni kilometa ngapi, mawanda yake ni mapana kiasi gani. Alipokuwa anaumba viumbe vyote, Aliamua pia mipaka ya majangwa, vilevile masafa ya vilima na uwiano wao, na vile vilivyopakana navyo—pia Aliamua yote haya. Aliamua mawanda ya mito na maziwa Alipokuwa anaviumba—vyote vina mipaka yao. Kwa hiyo ina maana gani tunaposema “mipaka”? Tulizungumza tu kuhusu ambavyo Mungu huongoza vitu vyote kwa kuanzisha sheria kwa vitu vyote. Yaani, masafa na mipaka ya milima havitaongezeka au kupungua kwa sababu ya mzunguko wa dunia au muda kupita. Hizi ni thabiti, hazibadiliki na ni Mungu ambaye huamrisha kutobadilika kwayo. Kwa maeneo ya tambarare, masafa yao, kile kilichopakana nayo, hii imewekwa na Mungu. Yana mipaka, na tuta haliwezi kutokea tu bila

mpangilio, katikati ya tambarare. Tambarare haiwezi tu kubadilika na kuwa mlima—hii haitatokea. Sheria na mipaka tuliyoizungumzia inarejelea hili. Kwa jangwa, hatutataja wajibu wa jangwa au mandhari nyingineyo au eneo la kijiografia hapa, ni mipaka yake tu. Chini ya kanuni ya Mungu mawanda ya jangwa nayo pia hayatapanuka. Hii ni kwa sababu Mungu amelipatia sheria yake, mawanda yake. Eneo lake ni kubwa kiasi gani na wajibu wake ni upi, kile kilichopakana nalo, na lipo mahali gani—hii imeshawekwa na Mungu tayari. Halitazidisha mawanda yake, kuhamisha sehemu yake, na halitaongeza eneo lake kiholela tu. Ingawa mtiririko wa maji kama vile mito na maziwa yote yapo katika mpangilio na mwendelezo, hayajawahi kwenda nje ya mawanda yao au kwenda zaidi ya mipaka yao. Yote yanafuata mwelekeo mmoja kwa namna ya mpangilio, yakitiririka kuelekea mwelekeo yanaopaswa kwenda. Kwa hiyo chini ya sheria ya kanuni ya Mungu, hakuna mto au ziwa ambalo litakauka kiholela tu, au kubadilisha mwelekeo au kiwango cha kutiririka kwake kiholela tu kwa sababu ya mzunguko wa dunia au kupita kwa muda. Hii yote ipo ndani ya maarifa ya Mungu. Hiyo ni sawa na kusema, vitu vyote vilivyoundwa na Mungu miongoni akiwemo binadamu, vina sehemu zao, maeneo yao, na mipaka yao. Yaani, Mungu alipoviumba viumbe vyote, mipaka yao ilianzishwa na hii haiwezi kugeuzwa kiholela tu, kufanywa upya au kubadilishwa. “Kiholela” inamaanisha nini? Ina maana kwamba havitahama, kupanuka, au kubadilisha umbo lao asilia bila mpangilio kwa sababu ya hali ya hewa, halijoto, au kasi ya mzunguko wa dunia. Kwa mfano, mlima una kimo fulani, kitako chake ni cha eneo fulani, una mwinuko fulani, na una kiasi fulani cha uoto. Hii yote imepangwa na kukokotolewa na Mungu na haitabadilishwa kiholela. Kwa tambarare, idadi kubwa ya binadamu wanaishi katika tambarare, na hakuna mabadiliko ya hali ya hewa yatakayoathiri maeneo yao au thamani ya uwepo wao. Sio hata kile ambacho kimejumuishwa katika mandhari haya na mazingira ya kijiografia ambayo yaliundwa na Mungu yatabadilika kiholela. Kwa mfano, vipengele vya jangwa ni vipi, ni aina gani ya madini yaliyopo chini ya ardhi, yanajumuisha mchanga kiasi gani na rangi ya mchanga, upana wake—haya hayatabadilika kiholela. Kwa nini hayatabadilika kiholela? Ni kwa sababu ya kanuni ya Mungu na usimamizi Wake. Ndani ya mandhari haya yote tofautitofauti na mazingira ya kijiografia yaliyoundwa na Mungu, Anasimamia kila kitu kwa njia iliyopangwa na kwa mpangilio. Kwa hiyo mazingira haya yote ya kijiografia bado yapo kwa miaka elfu kadhaa, makumi elfu ya miaka baada ya kuwa yameundwa na Mungu. Bado yanatimiza kila wajibu wao. Ingawa wakati wa vipindi fulani volkano hulipuka, wakati wa vipindi fulani matetemeko ya ardhi hutokea, na kuna mabadiliko makubwa ya ardhi, hakika Mungu hataruhusu aina yoyote ya mandhari kupoteza kazi yake ya asili. Ni kwa sababu tu ya usimamizi huu unaofanywa na Mungu, utawala Wake na udhhibiti wa sheria hizi, kwamba yote haya—yote haya yanayofurahiwa na binadamu na kuonwa na binadamu—yanaweza kuendelea kuishi duniani kwa njia ya mpangilio. Sasa kwa nini Mungu anasimamia mandhari yote haya yaliyopo duniani kwa njia hii? Kusudi ni ili viumbe hai

vinavyoendelea kuishi katika mazingira mbalimbali ya kijiografia yote yatakuwa na mazingira imara, na kwamba wataweza kuendelea kuishi na kuongezeka katika mazingira hayo imara. Vitu hivi vyote—vile vinavyotembea na vile ambavyo havitembei, vile ambavyo vinapumua kupitia mapua yao na vile ambavyo havitumii mapua—vinaunda mazingira ya tofauti kabisa kwa ajili ya binadamu kuendelea kuishi. Ni aina hii tu ya mazingira ndiyo inaweza kulea kizazi baada ya kizazi cha binadamu, na ni aina hii tu ya mazingira inaweza kuruhusu binadamu kuendelea kuishi kwa amani, kizazi baada ya kizazi.

Yale nimetoka tu kuyazungumzia ni mada kubwa kiasi, kwa hivyo labda inaonekana imeondolewa maishani mwenu, lakini naamini nyote mnaweza kuyaelewa, sivyo? Yaani, sheria za Mungu katika utawala wake wa vitu vyote ni muhimu sana—muhimu sana! Je, masharti ya awali ni yapi kwa viumbe vyote kukua ndani ya sheria hizi? Ni kwa sababu ya kanuni ya Mungu. Ni kwa sababu ya kanuni Yake ndipo vitu vyote vinafanya kazi zao ndani ya kanuni Yake. Kwa mfano, milima inalea misitu, halafu misitu inalea na kuwalinda ndege mbalimbali na wanyama wanaoishi ndani yake. Tambarare ni jukwaa lililoandaliwa kwa ajili ya binadamu kupanda mazao vilevile kwa ajili ya ndege na wanyama mbalimbali. Zinaruhusu idadi kubwa ya binadamu kuishi katika ardhi tambarare na kutoa hali isiyo na taabu katika maisha ya binadamu. Na tambarare pia zinajumuisha ukanda wa mbuga—malundo ya ukanda wa mbuga. Ukanda wa mbuga ni uoto wa nchi. Unalinda ardhi na kuwalea ng’ombe, kondoo na farasi wanaoishi katika ukanda wa mbuga. Jangwa pia linafanya kazi yake. Sio sehemu kwa ajili ya binadamu kuishi; jukumu lake ni kufanya hali ya hewa ya unyevunyevu kuwa kavu. Mitiririko ya mito na maziwa kunaleta hali isiyo ya usumbufu kwa ajili ya watu kunywa maji. Mahali popote yanapotiririka, watu watakuwa na maji kwa ajili ya kunywa, na mahitaji ya maji ya vitu vyote yataridhishwa kwa urahisi. Hii ni mipaka iliyochorwa na Mungu kwa ajili ya mandhari mbalimbali.

Kwa sababu ya mipaka hii ambayo Mungu ameichora, mandhari mbalimbali yamezalisha mazingira tofautitofauti kwa ajili ya binadamu kuendelea kuishi, na mazingira haya kwa ajili ya kuendelea kuishi yamekuwa na hali isiyokuwa na usumbufu kwa ajili ya aina tofautitofauti ya ndege na wanyama na vilevile kuleta nafasi kwa ajili ya kuendelea kuishi. Kutokana na hili, mipaka kwa mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa viumbe hai mbalimbali imeendelezwa. Hii ndiyo hoja ya pili tutakayokwenda kuzungumzia baadaye. Kwanza kabisa ni aina gani ya mazingira ambamo ndege na wanyama na wadudu wanaishi? Je, wanaishi katika misitu na vijisitu? Haya ndiyo makazi yao. Kwa hivyo, kando na kuanzisha mipaka kwa ajili ya mazingira mbalimbali ya kijiografia, Mungu pia Aliweka mipaka kwa ajili ya ndege na wanyama, samaki, wadudu mbalimbali, na mimea yote. Pia alianzisha sheria. Kwa sababu ya tofauti za mazingira mbalimbali ya kijiografia na kwa sababu ya uwepo wa mazingira tofauti ya kijiografia, aina tofautitofauti za ndege na wanyama, samaki, wadudu, na mimea vina mazingira tofauti kwa ajili

ya kuendelea kuishi. Ndege na wanyama na wadudu wanaishi miongoni mwa mimea, samaki wanaishi majini, na mimea inakua kwenye nchi kavu. Nchi kavu inajumuisha maeneo mbalimbali kama vile milima, tambarare, na vilima. Punde tu ndege na wanyama wanapokuwa na makazi yao yasiyobadilika, hawataweza kuzungukazunguka wakielekea njia yeyote. Makazi yao ni misitu na milima. Ikiwa, siku moja makazi yao yataharibiwa, mpangilio utakuwa machafuko. Mara tu mpangilio huo unapokuwa machafuko, madhara yake ni yapi? Wa kwanza kuumizwa ni akina nani? (Binadamu.) Ni binadamu. Ndani ya sheria na mipaka hii ambayo Mungu ameianzisha, je, mmewahi kuona tukio lolote la ajabu? Kwa mfano, tembo wakitembea jangwani kwa kawaida. Mmewahi kuona tukio hilo? Kama ingekuwa hivyo, lingekuwa ni tukio la ajabu sana, kwa sababu tembo wanaishi msituni, na ni mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo Mungu aliwaandalia. Wana mazingira yao wenyewe kwa ajili ya kuendelea kuishi na wana makazi yao yasiyobadilika, sasa kwa nini watangetange? Je, kuna mtu yeyote ambaye amewahi kuona simba au duma wakitembea ufuoni? Hapana, hamjawahi. Makazi ya simba na duma ni msituni na kwenye milima. Je, kuna mtu yeyote ambaye amewahi kumwona nyangumi au papa wa bahari akiogelea kupitia jangwani? Hakuna ambaye ameona hayo, siyo? Nyangumi na papa makazi yao ni baharini. Katika mazingira ya kuishi ya binadamu, je, kuna watu ambao wanaishi pamoja na dubu wa kahawia? Je, kuna watu ambao siku zote wamezungukwa na tausi au ndege wengineo, ndani au nje ya makazi yao? Je, kuna yeyote ambaye amewahi kuwaona tai au bata bukini wa mwituni wakicheza na tumbili? (Hakuna.) Haya yatakuwa ni matukio ya pekee sana. Sababu Ninazungumza juu ya vitu hivi ambavyo vinaonekana kuwa vya kipekee masikioni mwenu ni kuwafanya muelewe kwamba vitu vyote vilivyoubwa na Mungu—haijalishi kama vimewekwa katika sehemu moja au iwapo vinapumua kupitia mapuani—vina sheria zao kwa ajili ya kuendelea kuishi. Zamani kabla Mungu hajaumba viumbe hai hivi Alikuwa ameviandalia makazi yao, mazingira yao kwa ajili ya kuendelea kuishi. Viumbe hai hivi vilikuwa na mazingira yao yasiyobadilika kwa ajili ya kuendelea kuishi, chakula chao, makazi yao yasiyobadilika, sehemu zao zisizobadilika zinazowafaa kwa ajili ya kuendelea kuishi, maeneo yenye halijoto inayowafaa kwa ajili ya kuendelea kuishi. Kwa njia hiyo wasingezungukazunguka au kuhafifisha hali ya mwanadamu kuendelea kuishi au kuathiri maisha yao. Hivi ndivyo Mungu anavyoongoza vitu vyote, akiwaandalia wanadamu mazingira mazuri kabisa kwa ajili ya kuendelea kuishi. Viumbe hai chini ya vitu vyote kila kimoja kina chakula chao kinachokimu maisha yao wenyewe ndani ya mazingira yao wenyewe kwa ajili ya kuendelea kuishi. Kwa chakula hicho, vinajifunga katika mazingira yao ya asili kwa ajili ya kuendelea kuishi. Katika aina hiyo ya mazingira bado vinaendelea kuishi, kuzaliana, na kuendelea kulingana na sheria za Mungu alizozianzisha kwa ajili yao. Kwa sababu ya aina hizi za sheria, kwa sababu ya majaaliwa ya Mungu, vitu vyote vinaishi kwa upatanifu na wanadamu, na wanadamu huishi pamoja na vitu vyote kwa kutegemeana.

Mungu aliviumba vitu vyote na akaanzisha mipaka kwa ajili yao; miongoni mwao Akalea aina zote za viumbe hai. Wakati huo, pia Aliandaa mbinu tofauti kwa ajili ya binadamu kuendelea kuishi, hivyo unaweza kuona kwamba binadamu hawana njia moja tu kwa ajili ya kuendelea kuishi. Pia hawana aina moja tu ya mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi. Hapo kabla tulizungumza juu ya Mungu kuandaa aina mbalimbali za chakula na vyanzo vya maji kwa ajili ya binadamu, kitu ambacho ni muhimu sana kufanya uhai wa binadamu katika mwili kuendelea. Hata hivyo, miongoni mwa binadamu huyu, sio watu wote wanaishi kwa kula nafaka. Watu wana mbinu tofautitofauti za kuendelea kuishi kwa sababu ya tofauti za mazingira ya kijiografia na mandhari. Mbinu hizi za kuendelea kuishi zote zimeandaliwa na Mungu. Hivyo si binadamu wote wanajihusisha na kilimo. Yaani, si watu wote wanapata chakula chao kwa kulima mazao. Hii ni hoja ya tatu ambayo tutakwenda kuizungumzia. Mipaka imetengenezwa kutokana na mitindo mbalimbali ya maisha ya binadamu. Kwa hiyo ni aina nyingine ipi ya mtindo wa maisha ambayo binadamu wanayo? Kwa suala la vyanzo tofauti vya vyakula, ni aina gani nyingine ya vyakula ambavyo wanadamu wanavyo? Kuna aina za msingi kadhaa.

Ya kwanza ni mtindo wa maisha wa uwindaji. Kila mmoja anajua hiyo ni nini. Watu wanaoishi kwa kuwinda wanakula nini? (Windo.) Wanakula ndege na wanyama wa mwituni. “Windo” ni neno la kisasa. Wawindaji hawaoni kwamba ni mchezo, wanaona kama chakula, kama riziki yao ya kila siku. Kwa mfano, wangepata paa. Wanapopata paa huyu ni sawa tu na mkulima kupata mazao kutoka ardhini. Mkulima hupata mazao kutoka ardhini, na anapoona mazao yake anakuwa na furaha na anahisi amani. Familia haitakuwa na njaa ya mazao ya kula. Moyo wake una amani na anahisi kuridhika. Na mwindaji pia anahisi amani na kuridhika akiangalia kile ambacho amekamata kwa sababu hana haja ya kuwa na wasiwasi tena kuhusu chakula. Kuna kitu cha kula kwa ajili ya mlo unaofuata, hakuna haja ya kuwa na njaa. Huyu ni mtu ambaye anawinda kwa ajili ya kuishi. Wengi wa wale ambao hutegemea uwindaji wanaishi katika misitu ya milima. Hawalimi. Sio rahisi kupata ardhi inayolimika hapo, kwa hiyo wanaishi kwa kutegemea viumbe hai mbalimbali, aina mbalimbali za mawindo. Hii ni aina ya kwanza ya mtindo wa maisha ambao ni tofauti na ule wa watu wa kawaida.

Aina ya pili ni mtindo wa maisha wa ufugaji. Je, wale ambao wanafuga kwa ajili ya kuishi wanalima? (La.) Kwa hiyo sasa wanafanya nini? Wanaishije? (Kwa sehemu kubwa, wanafuga ng’ombe na kondoo kwa ajili ya kuishi, na msimu wa baridi wanawachinja na kuwala mifugo wao. Chakula chao cha msingi ni nyama ya ng’ombe na nyama ya kondoo, na wanakunywa chai ya maziwa. Ingawa wafugaji ni wenye shughuli misimu yote minne, wanakula vizuri. Wana kiwango kikubwa cha maziwa, bidhaa za maziwa, na nyama.) Watu wanaofuga mifugo kwa ajili ya kuishi kimsingi hula nyama ya ng’ombe na nyama ya kondoo, hunywa maziwa ya kondoo na ng’ombe, na wanaendesha madume ya ng’ombe na farasi uwandani na upepo kwenye nywele

zao, jua usoni pao. Hawana msongo wa mawazo juu ya maisha ya kisasa. Siku nzima wanaona tu upana wa wingu la bluu na tambarare za majani. Wengi wa watu wanaofuga mifugo kwa ajili ya kuishi wanaishi kwenye uwanda wa mbuga na wanaweza kuendelea na mtindo wao wa maisha ya kuhamahama kwa kizazi baada ya kizazi. Ingawa maisha katika uwanda wa mbuga ni ya upweke kidogo, pia ni maisha ya furaha. Si mtindo mbaya wa maisha!

Aina ya tatu ni mtindo wa maisha ya uvuvi. Kuna sehemu ndogo ya binadamu wanaoishi pembezoni mwa bahari au kwenye visiwa vidogo. Wamezungukwa na maji, wakikabiliana na bahari. Watu hawa huvua kwa ajili ya kuishi. Ni nini chanzo cha chakula kwa wale wanaovua kwa ajili ya kuishi? Vyanzo vyao vya vyakula ni pamoja na aina zote za samaki, vyakula vya baharini, na mazao mengine ya baharini. Watu wanaovua kwa ajili ya kuishi hawalimi mashamba, lakini badala yake wao huenda kuvua kila siku. Chakula chao cha msingi kinajumuisha aina mbalimbali za samaki, na bidhaa za vyakula vya baharini. Mara chache waliweza kubadilishana bidhaa hizi na mchele, unga, na mahitaji ya kila siku. Huu ni mtindo tofauti wa maisha wa watu wanaoishi karibu na maji. Wale wanaoishi karibu na maji wanayategemea kwa ajili ya chakula chao, na uvuvi ni riziki yao. Ni chanzo cha riziki yao vilevile chanzo chao cha chakula.

Licha ya wale ambao hulima kwa ajili ya kuishi, kimsingi kuna aina tatu tofauti za mtindo wa maisha zilizotajwa hapo juu. Licha ya wale ambao wanaishi kwa kutegemea ufugaji, uvuvi, na kuwinda, idadi kubwa ya watu hulima kwa ajili ya chakula. Na watu wanaolima kwa ajili ya kuishi wanahitaji nini? Wanahitaji udongo. Wao wanategemea kupanda mazao kwa vizazi. Haijalishi wanapanda mbogamboga, matunda au nafaka, wanapata chakula chao na mahitaji yao ya kila siku kutoka ardhini.

Masharti ya msingi kwa mitindo tofauti ya maisha ya binadamu ni yapi? Je, hayahitaji utunzaji wa msingi wa mazingira yao kwa ajili ya kuendelea kuishi? Yaani, ikiwa wale wanaotegemea uwindaji wangepoteza misitu ya milima au ndege na wanyama, chanzo cha riziki yao kingepotea. Mwelekeo ambao kabila hili na watu wa aina hii wanapaswa kuchukua ungekuwa wa mashaka, na hata huenda wakatoweka. Na wale ambao wanafuga kwa ajili ya riziki yao hutegemea nini? Kile ambacho kweli wanakitegemea si mifugo yao, lakini ni mazingira ambayo mifugo wao wanaendelea kuishi—uwanda wa mbuga. Kama kusingekuwa na uwanda wa mbuga, wangelishia wapi mifugo wao? Kondoo na ng'ombe wangekula nini? Bila mifugo, watu wanaohamama hawangukuwa na riziki. Bila chanzo cha riziki yao, watu hawa wangekwenda wapi? Kuendelea kuishi kungekuwa vigumu sana; wasingekuwa na maisha ya baadaye. Bila vyanzo vya maji, mito na maziwa yangekauka. Je, samaki hao wote wanaotegemea maji kwa ajili ya maisha yao wangeendelea kuwepo? Samaki hao wasingendelea kuishi. Je,

watu hao ambao wanategemea maji na samaki kwa ajili ya riziki yao wangeendelea kuishi? Ikiwa hawakuwa na chakula, ikiwa hawakuwa na chanzo cha riziki zao, watu hao wasingeweza kuendelea kuishi. Yaani, kama kuna tatizo na riziki zao au kuendelea kwao kuishi, jamii hizo zisingeendelea kuwepo. Zisingeweza kuendelea kuishi, na zingeweza kupotea, kufutiliwa mbali kutoka duniani. Na ikiwa wale ambao wanalima kwa ajili ya riziki yao wangepoteza ardhi yao, kama hawangeweza kupanda vitu, na kupata vyakula vyao kutoka kwa mimea mbalimbali, matokeo yake yangukuwa nini? Bila chakula, je, watu wasingekufa kwa njaa? Ikiwa watu wangukufa kwa njaa, je, aina hiyo ya watu isingefutiliwa mbali? Kwa hiyo hili ni kusudi la Mungu katika kudumisha mazingira mbalimbali. Mungu ana kusudi moja tu katika kudumisha mazingira mbalimbali na mifumo ya ikolojia, kudumisha viumbe hai tofautitofauti ndani ya kila mazingira—ni kulea aina zote za watu, kuwalea watu pamoja na maisha katika mazingira ya kijiografia tofautitofauti.

Ikiwa vitu vyote vya uumbaji vingepoteza sheria zao, visingeshi tena; ikiwa sheria za vitu vyote zingekuwa zimepotea, basi viumbe hai miongoni mwa vitu vyote visingeweza kuendelea. Wanadamu pia wangepoteza mazingira yao kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo wanayategemea kwa ajili ya kuendelea kuishi. Ikiwa binadamu wangepoteza hayo yote, wasingeweza kuendelea kuishi na kuongezeka kizazi baada ya kizazi. Sababu ya wanadamu kuendelea kuishi mpaka sasa ni kwa sababu Mungu amewapatia wanadamu viumbe vyote vya uumbaji kuvilea, kuwalea wanadamu kwa namna tofauti. Ni kwa sababu tu Mungu anawalea binadamu kwa namna tofauti ndio maana wameendelea kuishi mpaka sasa, kwamba wameendelea kuishi hadi siku ya leo. Kwa aina hiyo ya mazingira yasiyobadilika kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo ni ya kufaa na yapo katika mpangilio, aina zote za watu duniani, aina zote za jamii zinaweza kuishi ndani ya mawanda yao husika. Hakuna anayeweza kwenda zaidi ya mawanda haya au mipaka hii kwa sababu ni Mungu ambaye ameichora. Kwa nini Mungu aichore kwa namna hii? Hii ni muhimu sana kwa binadamu wote—ni muhimu sana! Mungu alichora mawanda ya kila aina ya kiumbe hai na aliweka mbinu ya kuendelea kuishi kwa kila aina ya binadamu. Pia aligawanya aina mbalimbali za watu na jamii mbalimbali duniani na akaweka mawanda yao. Hiki ndicho tunachotaka kujadili wakati ujao.

Nne, Mungu alichora mipaka kati ya jamii za rangi tofautitofauti. Duniani kuna watu weupe, watu weusi, watu wa kahawia na watu wa njano. Hawa ni aina tofauti za watu. Mungu pia aliweka mawanda kwa ajili ya maisha ya aina hizi tofauti za watu, na bila kutambua, watu wanaishi ndani ya mazingira yao stahiki kwa kuendelea kuishi chini ya usimamizi wa Mungu. Hakuna anayeweza kwenda nje ya hapa. Kwa mfano, wazungu, ni maeneo gani ambayo wanaishi kwa kiasi kikubwa? Kwa kiasi kikubwa wanaishi Ulaya na Marekani. Watu weusi kimsingi wanaishi Afrika. Na watu wa rangi ya kahawia wanaishi ndani ya eneo gani? Hasa

wanaishi Kusini-mashariki mwa Asia na Asia Kusini, kama vile Tailandi, Bara Hindi, Myanmar, Vietnam na Laos. Watu wenye rangi ya hudhurungi kimsingi wanaishi Asia, yaani, China, Japan, Korea ya Kusini na nchi nyinginezo kama hizo. Mungu amegawanya aina hizi tofautitofauti za jamii kwa usawa kiasi kwamba jamii hizi tofautitofauti zimegawanywa katika sehemu tofautitofauti za dunia. Katika sehemu tofautitofauti hizi za dunia, Mungu aliandaa zamani sana mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi yanayofaa kwa ajili ya kila jamii tofauti ya binadamu. Ndani ya aina hizi za mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi, Mungu amewaandalia rangi na vijenzi vya udongo. Kwa maneno mengine, vijenzi katika miili ya watu weupe havifanani na vile vilivyo ndani ya miili ya watu weusi, na pia ni tofauti na vijenzi vya miili ya watu wa jamii nyinginezo. Mungu alipoumba vitu vyote, tayari Alikuwa ameandaa mazingira ya namna hiyo kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa jamii hiyo. Lengo Lake katika hili lilikuwa kwamba pale ambapo aina hiyo ya watu inanza kuongezeka, watakapoanza kuongezeka kwa idadi, wangeweza kuwekwa ndani ya mawanda hayo. Kabla Mungu hajawaumba binadamu alikuwa amekwishatafakari yote—Angeweza kutoa Ulaya na Amerika kwa watu weupe na kuwaruhusu kuliendeleza na kuendelea kuishi. Kwa hiyo Mungu alipokuwa anatengeneza dunia tayari Alikuwa na mpango, alikuwa na nia na kusudi katika kile alichokuwa anakiweka katika kipande hicho cha ardhi, na kile ambacho kingelelewa katika kipande hicho cha ardhi. Kwa mfano, Mungu zamani sana aliandaa mlima upi, tambarare ngapi, vyanzo vya maji vingapi, ni aina gani ya ndege na wanyama, samaki gani, na mimea gani ingeweza kuwepo katika ardhi hiyo. Alipokuwa anaandaa mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa ajili ya aina ya binadamu, kwa ajili ya jamii, Mungu aliangalia vipengele vingi vya masuala: mazingira ya kijiografia, vijenzi vya udongo, aina ya ndege na wanyama, ukubwa wa aina tofautitofauti za samaki, vijenzi katika samaki, ubora tofauti wa maji, vilevile aina tofauti za mimea.... Mungu alikuwa ameandaa yote hayo zamani sana. Mazingira ya aina hiyo ni mazingira ya asili kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo Mungu aliyaumba na kuyaandaa kwa ajili ya watu weupe na kwa hivyo ni yao kiasili. Mmeweza kuona kwamba Mungu alipoviumba vitu vyote Alitafakari sana na Alitenda kwa mpango? (Ndiyo, tumeona kwamba fikira za Mungu kwa aina mbalimbali za watu zilikuwa ni za uangalifu sana. Kwa mazingira aliyoyaumba kwa ajili ya kuendelea kuishi kwa ajili ya aina tofautitofauti za binadamu, aliandaa aina za ndege na wanyama na aina za samaki, milima mingapi na tambarare ngapi zitakuwepo. Yote haya yalifikiriwa kwa uangalifu sana na kwa usahihi.) Kwa mfano, vyakula wanavyokula wazungu hasa ni vipi? Vyakula ambavyo watu weupe wanakula ni tofauti sana na vyakula ambavyo watu wa Asia wanakula. Vyakula vikuu ambavyo watu weupe wanakula hasa ni nyama, mayai, maziwa, na kuku. Nafaka kama vile mkate na mchele kwa ujumla sio chakula kikuu ambacho kinawekwa pembeni mwa sahani. Hata pale wanapokula kachumbari ya mboga, wanaweka kiasi cha nyama ya kukaanga au kuku ndani yake. Hata kama wanakula vyakula vinavyotokana na ngano, wanaongeza siagi, mayai, au

nyama kwenye chakula hicho. Hiyo ni kusema, vyakula vyao vikuu havijumuishi hasa vyakula vinavyotokana na ngano au mchele; wanakula sana nyama na siagi. Mara nyingi wanakunywa maji ya barafu kwa sababu wanakula vyakula vyenye kalori ya juu sana. Kwa hiyo watu weupe ni wenye afya kweli. Hivi ndivyo vyanzo vya maisha yao, mazingira yao kwa ajili ya kuishi yaliandaliwa na Mungu kwa ajili yao, yanawafanya wawe na aina hiyo ya mtindo wa maisha. Mtindo huo wa maisha ni tofauti na mitindo ya maisha ya watu wa jamii nyingine. Hakuna baya au zuri katika mtindo huu wa maisha—ni wa kuzaliwa, uliamuliwa kabla na Mungu na kwa sababu ya kanuni ya Mungu na mipangilio Yake. Aina hii ya mbari ina mtindo fulani wa maisha na vyanzo fulani vya riziki zao kitu ambacho ni kwa sababu ya mbari yao, vilevile ni kwa sababu ya mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi yaliyoandaliwa na Mungu kwa ajili yao. Mngeweza kusema kwamba mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo Mungu aliyaandaa kwa ajili ya watu weupe na chakula cha kila siku wanachokipata kutoka katika mazingira hayo ni kingi na kimejaa tele.

Mungu pia aliandaa mazingira yanayofaa kwa ajili ya mbari nyingine kuendelea kuishi. Pia kuna watu weusi—watu weusi wanapatikana wapi? Hasa wanapatikana katikati na kusini mwa Afrika. Mungu aliwaandalia nini kwa ajili ya kuishi katika aina hiyo ya mazingira? Misitu ya kitropiki, aina zote za ndege na wanyama, pia majangwa, na aina zote za mimea ambayo inaambatana nao. Wana vyanzo vya maji, riziki zao, na chakula. Mungu hakuwabagua. Bila kujali kile walichowahi kukifanya, kuendelea kuishi kwao hakujawahi kuwa tatizo. Pia wanachukua mahali fulani maalumu na eneo fulani katika sehemu ya dunia.

Sasa, hebu tuzungumze kidogo kuhusu watu wa njano. Watu wa njano hasa wanapatikana nchi za Mashariki. Kuna tofauti gani kati ya mazingira na sehemu za kijiografia za nchi za Mashariki na nchi za Magharibi? Katika nchi za Mashariki, eneo kubwa la ardhi ni la rutuba, na zina hazina kubwa ya vitu na madini. Yaani, aina zote za rasilimali za juu ya ardhi na za chini ya ardhi zimejaa tele. Na kwa kundi hili la watu, kwa mbari hii, Mungu pia aliandaa udongo, hali ya hewa inayofanana nao, na mazingira mbalimbali ya kijiografia ambayo yanawafaa. Ingawa kuna tofauti kubwa kati ya mazingira hayo ya kijiografia na mazingira ya nchi za Magharibi, chakula cha lazima cha watu, riziki, na vyanzo kwa ajili ya kuendelea kuishi viliandaliwa na Mungu. Ni mazingira tofauti tu kwa ajili ya kuishi kuliko yale ambayo watu weupe wanayo katika nchi za Magharibi. Lakini ni kitu kipi kimoja ambacho Ninahitaji kuvuta usikivu wenu, ambacho Ninahitaji kuwaambia? Idadi ya mbari ya Mashariki kiasi fulani ni kubwa, hivyo Mungu aliongeza vipengele vingi katika kipande hicho cha ardhi ambavyo ni tofauti na vya Magharibi. Katika upande huo wa dunia, Aliongeza mandhari mengi mbalimbali na aina zote za vitu vingi. Huko rasilimali za asili ni tele; mandhari pia yanatofautiana na anuwai, yanatosha kwa ajili ya kulea idadi kubwa ya mbari ya Mashariki. Kitu fulani ambacho ni tofauti na Magharibi ni

kwamba Mashariki—kutoka kusini kwenda kaskazini, kutoka mashariki kwenda magharibi—hali ya hewa ni nzuri kuliko ya Magharibi. Misimu minne imeoneshwa kinaganaga, hali ya joto ni nzuri, rasilimali za asili zipo tele, mazingira ya asili na aina za mandhari ni mazuri zaidi kuliko ya Magharibi. Kwa nini Mungu alifanya hivi? Mungu alitengeneza uwiano razini kabisa kati ya watu weupe na watu wa njano. Hii inamaanisha nini? Inamaanisha kuwa kila kipengele cha chakula chao, vitu ambavyo wanatumia, kile ambacho watu weupe wanacho cha kujifurahisha ni kizuri zaidi kuliko kile ambacho watu wa njano wanaweza kukifurahia. Hata hivyo, Mungu habagui mbari yoyote. Mungu aliwapatia watu wa njano mazingira mazuri na bora zaidi kwa ajili ya kuendelea kuishi. Hii ni uwiano.

Mungu amjalia kabla ni aina gani ya watu wanastahili kuishi katika sehemu ipi ya dunia; je, wanadamu wanaweza kupita hii mipaka? (La.) Kitu cha ajabu kweli! Hata kama kuna vita au uvamizi katika enzi mbalimbali au nyakati fulani, vita hivi, uvamizi huu, hakika hauwezi kuharibu mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo Mungu aliyaamua kabla kwa ajili ya kila mbari. Yaani, Mungu amewaweka aina fulani ya watu katika eneo fulani la dunia na hawawezi kwenda nje ya mawanda hayo. Hata kama watu wana lengo la kubadilisha au kuongeza eneo lao, bila ruhusa ya Mungu, hii itakuwa vigumu sana kufanikiwa. Itakuwa vigumu sana kufanikiwa. Kwa mfano, watu weupe walitaka kuongeza maeneo yao na wakazitawala kwa mabavu baadhi ya nchi. Wajerumani walivamia baadhi ya nchi, Uingereza waliitwaa India. Matokeo yalikuwa ni nini? Mwishowe walishindwa. Tunaona nini kutokana na kushindwa huku? Kile ambacho Mungu amekiamua kabla hakiwezi kuharibiwa. Kwa hiyo, haijalishi ni nguvu kubwa kiasi gani ambayo umeweza kuiona katika upanuzi wa Uingereza, mwishowe walitakiwa bado kuondoka, na kuacha ardhi hiyo ikiwa bado ni ya India. Wale ambao wanaishi katika ardhi hiyo bado ni Wahindi, na si Waingereza. Hii ni kwa sababu ni kitu ambacho Mungu haruhusu. Baadhi ya wale ambao wanatafiti historia au siasa wametoa tasnifu juu ya hili. Wanatoa sababu kwa nini Uingereza ilishindwa, wanasema kwamba pengine ilikuwa ni kwa sababu mbari fulani isingeweza kushindwa, au pengine ni kwa sababu ya sababu nyinginezo za kibinadamu.... Hizi sio sababu za kweli. Sababu ya kweli ni kwa sababu ya Mungu—Haruhusu hilo! Mungu anaamua mbari waishi katika nchi fulani na Anawaweka hapo, na kama Mungu hawaruhusu kuhama hawataweza kuhama kamwe. Ikiwa Mungu ataamua mawanda kwa ajili yao, wataishi ndani ya mawanda hayo. Binadamu hawezi kuvunja bure au kwenda nje ya mawanda haya. Hii ni hakika. Haijalishi nguvu za wavamizi ni kubwa kiasi gani, au jinsi gani wale wanaovamiwa ni dhaifu, mafanikio yao mwishowe yanamtegemea Mungu. Ameshaliamua hili tayari na hakuna anayeweza kulibadilisha.

Haya ya juu ndivyo Mungu alivyogawanya mbari mbalimbali. Ni kazi gani ambayo Mungu amefanya kuzigawanya mbari? Kwanza, aliandaa mazingira makubwa ya kijiografia, Akiwapa

watu maeneo tofautitofauti, na kisha kizazi baada ya kizazi kinaendelea kuishi pale. Hii imeamuliwa—mawanda ya kuendelea kuishi kwao yameamuliwa. Na maisha yao, kile wanachokula, kile wanachokunywa, riziki zao—Mungu aliamua hayo yote zamani sana. Na Mungu alipokuwa anaumba vitu vyote, Alifanya maandalizi tofautitofauti kwa ajili ya aina tofauti za watu: Kuna vijenzi tofautitofauti vya udongo, hali ya hewa tofauti, mimea tofauti, na mazingira tofauti ya kijiografia. Maeneo tofautitofauti yana hata ndege na wanyama tofauti, maji tofauti yana aina tofauti za samaki wao spesheli na bidhaa za majini. Hata aina ya wadudu inaamuliwa na Mungu. Kwa mfano, vitu ambavyo vinakua katika bara la Marekani vyote ni vikubwa sana, virefu sana na vyenye nguvu sana. Mizizi ya miti kwenye mlima wa msitu yote haina kina kirefu kabisa, lakini inakua mirefu sana. Inaweza kurefuka hadi kimo cha mita mia moja au zaidi, lakini miti katika misitu ya Asia kwa kiasi kikubwa siyo mirefu sana. Chukua mimea ya mshubiri kwa mfano. Nchini Japani, mimea hii ni midogo sana na miembamba sana, lakini mimea ya mshubiri nchini Marekani ni mikubwa mno. Hii ni tofauti. Ni aina ile ile ya mmea ikiwa na jina lile lile, lakini katika bara la Marekani ni kubwa hasa. Tofauti katika vipengele hivi tofautitofauti zinaweza zisionekane au kufahamika kwa watu, lakini Mungu alipokuwa anaumba vitu vyote, alivionyesha kinaganaga na aliandaa mazingira tofauti ya kijiografia, mandhari tofauti, na viumbe hai tofauti kwa ajili ya mbari mbalimbali. Hiyo ni kwa sababu Mungu aliumba aina tofautitofauti za watu, na Anajua kile ambacho kila mmoja anahitaji na mitindo yao ya maisha ni nini.

Baada ya kuzungumza juu ya baadhi ya vitu hivi, sasa mna uelewa fulani wa mada kuu ambayo tumeijadili hivi punde? Je, mmeielewa kwa kiasi fulani? Kuna sababu ambayo nimeongea kuhusu mambo haya ndani ya mada pana—sasa mnapaswa kuwa mmeielewa angalau kwa muhtasari, sivyo? Mnaweza kuniambia mmeielewa kwa kiasi gani. (Binadamu wote wameelewa kwa sheria ambazo ziliamuliwa na Mungu kwa ajili ya vitu vyote. Mungu alipokuwa anaamua sheria hizi, Aliandaa mbari tofautitofauti zikiwa na mazingira tofauti, mitindo tofauti ya maisha, vyakula tofauti, na hali ya hewa na halijoto tofauti. Hii ilikuwa hivyo ili binadamu wote waweze kuishi duniani na kuendelea kuishi. Kutokana na hili naweza kuona mipango ya Mungu ya kuendelea kwao kuishi yako dhahiri sana na ninaweza kuona hekima Yake na ukamilifu Wake, na upendo Wake kwa sisi binadamu.) (Sheria na mawanda yaliyoamuliwa na Mungu hayawezi kubadilishwa na mtu yeyote, tukio, au kitu. Yote ipo chini ya kanuni Yake.) Tukiangalia kwa mtazamo wa sheria zilizoamriwa na Mungu kwa ukuaji wa vitu vyote, yote hii si kwa ajili ya mwanadamu, haijalishi ni wa aina gani, anaishi chini ya uangalizi wa Mungu—je, wote hawaishi chini ya malezi Yake? Ikiwa sheria hizi zingeharibiwa au Mungu hakuanzisha aina hizi za sheria kwa ajili ya binadamu, majaliwa yao yangukuwa ni nini? Baada ya binadamu kupoteza mazingira yao ya msingi kwa ajili ya kuendelea kuishi, je,

wangukuwa na chanzo chochote cha chakula? Inawezekana kwamba vyanzo vya chakula vingekuwa tatizo. Ikiwa watu wangepoteza vyanzo vyao vya chakula, yaani, ikiwa hawangeweza kupata kitu chochote cha kula, ni siku ngapi wangeweza kuvumilia? Pengine wasingeweza kuvumilia hata kwa mwezi mmoja, na kuendelea kuishi kwao kungekuwa ni tatizo. Kwa hiyo kila kitu ambacho Mungu anafanya kwa ajili ya watu kuendelea kuishi, kwa ajili ya wao kuendelea kuwepo, kuongezeka, na ruzuku ni muhimu sana. Kila kitu ambacho Mungu anafanya miongoni mwa vitu vyote vinahusiana kwa karibu na haviwezi kutenganishwa na watu kuendelea kuishi. Ikiwa kuendelea kuishi kwa binadamu kulikuwa tatizo, je, usimamizi wa Mungu ungeweza kuendelea? Je, usimamizi wa Mungu bado ungekuwepo? Usimamizi wa Mungu unakwenda sambamba na kuendelea kuishi kwa binadamu wote ambao Anawalea, kwa hivyo haijalishi Mungu anaandaa kitu gani kwa ajili ya vitu vyote na kile Anachofanya kwa ajili ya binadamu, hii yote ndiyo lazima Kwake, na ni muhimu sana kwa ajili ya binadamu kuendelea kuishi. Ikiwa sheria zote hizi ambazo Mungu aliziamua kwa ajili ya vitu vyote zingekuwa zimeachwa, ikiwa sheria hizi zingekuwa zimevunjwa au zimeharibiwa, vitu vyote visingeweza kuwepo, mazingira ya binadamu ya kuendelea kuwepo yasingekuwepo, na wala riziki zao za kila siku, na wala wao wenyewe. Kwa sababu hii, Usimamizi wa Mungu wa wokovu wa binadamu wala nao usingekuwepo pia.

Kila kitu ambacho tumejadili, kila kitu, kila kipengele kimeungana kikamilifu na kuendelea kuishi kwa kila mtu. Mnaweza kusema, “Unachokizungumzia ni kikubwa sana, hatuwezi kukiona,” na pengine kuna watu ambao wangeweza kusema “Unachokizungumzia hakinihusu.” Hata hivyo, usisahau kwamba unaishi kama sehemu tu ya vitu vyote; wewe ni mshirika wa vitu vyote ndani ya kanuni ya Mungu. Vitu vyote haviwezi kutenganishwa na kanuni ya Mungu, na hakuna mtu hata mmoja ambaye anaweza kujitenganisha kwenye kanuni Yake. Kupoteza kanuni Yake na kupoteza uangalizi wake kungekuwa na maana kwamba maisha ya watu, maisha ya watu katika mwili yangetoweka. Huu ndio umuhimu wa Mungu kuanzisha mazingira kwa ajili ya binadamu kuendelea kuishi. Haijalishi wewe ni mbari gani au unaishi katika ardhi gani, iwe ni Magharibi au Mashariki—huwezi kujitenganisha na mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo Mungu ameyaanzisha kwa ajili ya binadamu, na huwezi kujitenga na malezi na uangalizi wa mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo Ameyaanzisha kwa ajili ya binadamu. Haijalishi riziki yako ni nini, kile unachokitegemea kwa ajili ya kuishi, na kile unachokitegemea kudumisha uhai wako katika mwili, huwezi kujitenganisha na kanuni ya Mungu na usimamizi wake. Baadhi ya watu wanasema: “Mimi sio mkulima, sipandi mazao kwa ajili ya kuishi. Sitegemei mbingu ili nipate chakula changu, kwa hiyo siendelei kuishi katika mazingira ambayo aliyaanzisha Mungu kwa ajili ya kuendelea kuishi. Aina hiyo ya mazingira haijanipatia kitu chochote.” Hii ni kweli? Unasema kwamba hupandi mazao kwa ajili ya kuishi,

lakini huli nafaka? Huli nyama na mayai? Je, huli mbogamboga na matunda. Kila kitu unachokula, vitu hivi vyote unavyovitaka havitenganishwi na mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi yaliyoanzishwa na Mungu kwa ajili ya binadamu. Na chanzo cha kila kitu ambacho binadamu anahitaji hakiwezi kutenganishwa na vitu vyote vilivyoundwa na Mungu, aina hizo za mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi. Maji unayokunywa, nguo unazovaa, na vitu vyote unavyotumia—ni kitu gani kati ya hivi ambacho hakipatikani kutoka katika vitu hivi vyote? Baadhi ya watu husema: “Kuna baadhi ya vitu ambavyo havipatikani kutoka katika vitu vyote hivi. Unaona, plastiki haitokani na vitu vyote hivi. Ni kitu cha kemikali, kitu kilichotengenezwa na mwanadamu.” Hii ni sahihi? Plastiki imetengenezwa na mwanadamu, ni kitu cha kemikali, lakini vijenzi asilia vya plastiki vilitoka wapi? Vijenzi asilia vilipatikana kutoka katika vitu ambavyo kwa asili vilitengenezwa na Mungu. Vitu ambavyo unavifurahia, ambavyo unaona, kila kitu ambacho unatumia, vyote vinapatikana kutoka katika vitu vyote ambavyo vilitengenezwa na Mungu. Hiyo ni sawa na kusema, haijalishi ni mbari gani, haijalishi ni riziki gani, au ni katika aina gani ya mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo watu wanaishi, hawawezi kujitenganisha na uungalizi wa Mungu. Kwa hiyo mambo haya tuliyoyajadili leo yanahusiana na mada yetu ya “Mungu ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote”? Je, vitu tulivyovijadili leo vinaangukia chini ya mada hii kubwa? (Ndiyo.) Pengine baadhi ya ambayo nimeyazungumzia leo ni ya kidhahania kidogo na ni vigumu kidogo kuweza kuyajadili. Hata hivyo, Nadhani kwamba sasa mnaelewa vizuri kidogo.

Nyakati chache hizi katika ushirika, kiwango cha mada ambazo tumekuwa nazo katika ushirika ni kipana sana, na mawanda yao ni mapana, kwa hiyo unapaswa uwe na jitihada kiasi fulani ili uweze kuzielewa zote. Hii ni kwa sababu mada hizi ni vitu ambavyo watu hawajawahi kukabiliana navyo katika imani yao kwa Mungu. Baadhi ya watu wanaisikia kama muujiza na baadhi ya watu wanaisikia kama hadithi—mtazamo gani ni sahihi? Unasikia haya yote kutoka katika mtazamo gani? (Tumeona jinsi Mungu amepanga vitu vyote kwa mbinu yenye mpangilio na kwamba vitu vyote vina sheria hizi na kupitia maneno haya tunaweza kuelewa zaidi juu ya matendo ya Mungu na mpangilio wake angalifu na sahihi kwa ajili ya kumwoko binadamu.) Kupitia nyakati hizi katika ushirika, Mmeona mawanda ya usimamizi wa Mungu wa vitu vyote ni nini? (Binadamu wote, kila kitu.) Je, Mungu ni Mungu wa mbari moja? Je, ni Mungu wa aina moja ya watu? Je, ni Mungu wa eneo dogo la binadamu? (Hapana, hayupo hivyo.) Kwa kuwa Hayupo hivyo, katika maarifa ya watu juu ya Mungu, ikiwa angekuwa ni Mungu wa sehemu ndogo tu ya binadamu, au ikiwa unaamini kwamba Mungu ni Mungu wako tu, je, mtazamo huu upo sahihi? Kwa kuwa Mungu anasimamia na kutawala vitu vyote, watu wanapaswa kuona matendo Yake, hekima Yake, na ukuu Wake ambavyo vimefunuliwa katika utawala Wake wa vitu vyote. Hiki ni kitu ambacho watu wanapaswa kufahamu. Ikiwa unasema kwamba Mungu

anasimamia vitu vyote, na Anatawala juu ya vitu vyote, lakini kama huna uelewa wowote au umaizi katika utawala Wake kwa binadamu, je, unaweza kutambua kwamba Anatawala vitu vyote? Unaweza kufikiri moyoni mwako, “Ninaweza, kwa sababu ninaona kwamba maisha yangu haya yote yanatawaliwa na Mungu.” Je, kweli Mungu ni mdogo kiasi hicho? Hayupo hivyo! Unaona tu wokovu wa Mungu kwa ajili yako na kazi yake kwako, na kutokana na vitu hivi unauona utawala Wake. Hayo ni mawanda finyu sana, na yana athari katika maarifa yako halisi juu ya Mungu. Pia yanaweka mipaka kwenye maarifa yako halisi juu ya utawala wa Mungu juu ya vitu vyote. Ikiwa unayawekea mipaka maarifa yako kuhusu Mungu kwenye mawanda ya kile ambacho Mungu anatoa kwa ajili yako na wokovu Wake kwa ajili yako, hutaweza kutambua kwamba anatawala kila kitu, kwamba anatawala vitu vyote, na anatawala binadamu wote. Unaposhindwa kutambua haya yote, je, kweli unaweza kutambua ukweli kwamba Mungu anatawala majaliwa yako? Huwezi. Moyoni mwako hutaweza kutambua kipengele hicho—hutoweza kutambua kiwango hicho. Uaelewa, siyo? Kwa kweli, Ninajua ni kwa kiwango gani mnaweza kuelewa mada hizi, maudhui haya ninayoyazungumzia, sasa kwa nini Naendelea kuizungumzia? Ni kwa sababu mada hizi ni mambo ambayo yanapaswa kueleweka kwa kila mfuasi wa Mungu, kila mtu ambaye anataka kuokolewa na Mungu— anapaswa kuelewa mada hizi. Ingawa, kwa kipindi hiki ambacho huzielewi, siku moja, ambapo maisha yako na uzoefu wako wa ukweli utafikia kiwango fulani, pale ambapo mabadiliko yako ya tabia yako ya maisha yanafikia kiwango fulani na kimo chako kinaongezeka kwa kiwango fulani, ni wakati huo tu ndio mada hizi ambazo naziwasilisha kwako katika ushirika zitakimu na kuridhisha utafutaji wako wa maarifa ya Mungu. Kwa hiyo maneno haya yalikuwa ni kwa ajili ya kuweka msingi, kuwaandaa kwa ajili ya uelewa wenu wa baadaye kwamba Mungu anatawala vitu vyote na kwa ajili ya uelewa wenu wa Mungu Mwenyewe.

Vyovyote vile uelewa juu ya Mungu ulivyo mkubwa katika mioyo ya watu, unaamua nafasi kubwa kiasi gani Anachukua katika mioyo yao. Vyovyote vile kiwango cha maarifa ya Mungu kilivyo katika mioyo yao ndivyo kwa kiwango kikubwa Mungu alivyo katika mioyo yao. Ikiwa Mungu unayemfahamu yupo tupu na ni yule asiye yakini, basi yule Mungu unayemwamini pia ni tupu na ni yule asiye yakini. Mungu unayemfahamu anaishia ndani ya mipaka ya upeo wa maisha yako binafsi, na hahusiani na Mungu wa kweli Mwenyewe. Kwa hiyo, kuyajua matendo ya Mungu, kuujua uhalisi wa Mungu na uweza Wake, kuujua utambulisho wa kweli wa Mungu Mwenyewe, kujua kile Anacho na alichokujua kile Alichokuonyesha miongoni mwa vitu vyote—haya ni muhimu sana kwa kila mtu anayetafuta maarifa ya Mungu. Haya yana uhusiano wa moja kwa moja na iwapo watu wanaweza kuingia kwa uhalisi wa ukweli. Ikiwa unauwekea mipaka uelewa wako juu ya Mungu katika maneno tu, ikiwa unauwekea mipaka uelewa wako mdogo tu, Neema ya Mungu unayoihesabu, au shuhuda zako ndogo kwa Mungu, basi Ninasema

kwamba yule Mungu unayemwamini si Mungu Mwenyewe wa kweli kabisa, na inaweza pia kusemwa kuwa Mungu unayemwamini ni Mungu wa fikira tu, si Mungu wa kweli. Hii ni kwa sababu Mungu wa kweli ni Yule ambaye Anatawala kila kitu, ambaye Anatembea miongoni mwa kila kitu, ambaye Anasimamia kila kitu. Yeye ndiye Anashikilia majaliwa ya binadamu wote—ambaye anashikilia majaliwa ya kila kitu. Kazi na matendo ya Mungu ambaye Ninamzungumzia hayaishii kwa sehemu ndogo tu ya watu. Yaani, haiishii tu kwa watu tu ambao sasa wanamfuata. Matendo Yake yameonyeshwa miongoni mwa vitu vyote, katika vitu vyote kuendelea kuishi, na katika sheria za mabadiliko ya vitu vyote.

Kama huwezi kuona au kutambua matendo yoyote ya Mungu kati ya vitu vyote, basi huwezi kutoa ushuhuda kwa matendo Yake yoyote. Ikiwa huwezi kuwa na ushuhuda wowote kwa Mungu, ikiwa unaendelea kuzungumza juu ya huyo anayeitwa Mungu mdogo ambaye unamfahamu, Mungu huyo ambaye anaishia kwenye mipaka ya mawazo yako tu, na yupo ndani ya akili yako finyu, ikiwa unaendelea kuzungumza juu ya aina hiyo ya Mungu, basi Mungu hataisifu imani yako. Unapokuwa na ushuhuda kwa ajili ya Mungu, ikiwa unatumia tu jinsi unavyofurahia neema ya Mungu, kukubali adhabu na kurudi Kwake, na kufurahia baraka Zake katika ushuhuda wako Kwake, ambao kwa kiasi kikubwa hautoshi na hauwezi kumridhisha. Ikiwa unataka kuwa na ushuhuda kwa ajili ya Mungu kwa namna ambayo inakubaliana na mapenzi Yake, kuwa na ushuhuda kwa Mungu Mwenyewe wa kweli, basi unapaswa kuona kile Mungu anacho na alichokutokana na matendo Yake. Unapaswa kuona mamlaka ya Mungu kutoka katika udhibiti Wake wa kila kitu, na kuona ukweli wa jinsi Anavyowakimu binadamu wote. Ikiwa unakiri tu kwamba chakula chako cha kila siku na kinywaji na mahitaji yako katika maisha yanatoka kwa Mungu, lakini huoni ukweli kwamba Mungu anawakimu binadamu wote kwa njia ya vitu vyote, kwamba anawaelekeza wanadamu, basi hutaweza kamwe kuwa na ushuhuda kwa ajili ya Mungu. Lengo Langu la kusema haya yote ni lipi? Iko hivyo ili usiweze kulichukulia hili kirahisi, ili msiamini kwamba mada hizi Nilizozitungumzia hazina uhusiano na kuingia kwenu binafsi katika maisha, na ili msichukue mada hizi kama tu aina ya maarifa au mafundisho. Ikiwa unasikiliza ukiwa na mtazamo kama huo, hutapata kitu hata kimoja. Mtapoteza fursa kubwa hii ya kumjua Mungu.

Lengo Langu la kuzungumza juu ya mambo haya yote ni nini? Lengo langu ni kuwafanya watu wamjue Mungu, kuwafanya watu waelewe matendo halisi ya Mungu. Mara utakapomuelewa Mungu na ukaelewa matendo Yake, ni baada ya hapo tu ndipo utakuwa na fursa au uwezekano wa kumjua Mungu. Kwa mfano, ikiwa unataka kumwelewa mtu, ni jinsi gani unaweza kumwelewa? Je, inaweza kuwa kupitia kuangalia umbo lao la nje? Je, inaweza kuwa kupitia kile wanachokivaa, jinsi wanavyovaa? Je, inaweza kuwa ni kupitia kuangalia jinsi wanavyotembea? Je, inaweza kuwa ni kupitia kuangalia mawanda ya maarifa yao? (Hapana.)

Kwa hiyo unamwelewaje mtu? Unafanya hukumu kupitia maneno na tabia ya mtu, kupitia mawazo zake, kupitia kile anachokionyesha na kile anachokifichua. Hivyo ndivyo unavyomjua mtu, unavyomwelewa mtu. Kwa njia ile ile, ikiwa mnahitaji kumjua Mungu, ikiwa mnataka kuelewa upande Wake wa vitendo, upande Wake wa kweli, mnapaswa kumjua Yeye kupitia matendo Yake na kupitika kila kitu halisi Anachofanya. Hii ndiyo njia bora zaidi na ndiyo njia pekee.

Mungu anaweka Uwiano Kati ya Vitu Vyote ili Kumpatia Binadamu Mazingira Imara kwa ajili ya Kuendelea Kuishi

Mungu anadhihirisha matendo Yake miongoni mwa vitu vyote na miongoni mwa vitu vyote Anavyovitawala na Anashikilia sheria za vitu vyote. Tumemaliza kusema juu ya jinsi ambavyo Mungu anatawala sheria za vitu vyote vilevile jinsi ambavyo Anawakimu na kuwalea binadamu wote ndani ya sheria hizo. Hiki ni kipengele kimoja. Kinachofuata, tutazungumza juu ya kipengele kingine, ambacho ni njia moja ambayo Mungu ana udhibiti wa kila kitu. Hivi ndivyo, baada ya kuumba vitu vyote, Akaweka uwiano wa uhusiano kati yao. Hii pia ni mada kubwa sana kwenu. Kuweka uwiano wa uhusiano kati ya vitu vyote—je, hiki ni kitu ambacho watu wanaweza kufanya? Binadamu wenyewe hawawezi. Watu wanaweza tu kuharibu. Hawawezi kuweka uwiano wa uhusiano kati ya vitu vyote; hawawezi kuvisimamia, wala hawana mamlaka makubwa hayo au nguvu. Ni Mungu Mwenyewe ndiye ana aina ya nguvu kuweza kufanya kitu cha aina hii. Kusudi la Mungu la kufanya kitu cha aina hii—kinamsaidia nini? Ni vilevile, inafanana kwa ukaribu na kuendelea kuishi kwa binadamu. Kila kitu ambacho Mungu anataka kufanya ni cha lazima—hakuna kitu ambacho Anaweza au asiweze kufanya. Ili Yeye alinde kuendelea kuishi kwa binadamu na kuwapatia watu mazingira yanayofaa kwa ajili ya kuendelea kuishi, kuna vitu fulani vya lazima, vitu fulani vya muhimu sana ambavyo ni lazima Afanye kulinda kuendelea kuishi kwao.

Kutokana na maana ya moja kwa moja ya kirai “Mungu anaweka uwiano kwa vitu vyote,” ni mada pana sana; kwanza inakupatia dhana ili uweze kujua kwamba kuweka uwiano kwa vitu vyote ni utawala wa Mungu kwa vitu vyote. Neno hili “uwiano” linamaanisha nini? Kwanza, “uwiano” unamaanisha kutoruhusu kitu fulani kutoka nje ya uwiano. Ni kama kutumia mizani kupima vitu. Ili kuweka uwiano kwenye mizani, uzito wa kila upande lazima uwe sawa. Mungu aliumba vitu vingi miongoni mwa vitu vyote—Aliumba vitu ambavyo havibadiliki, vitu ambavyo vinajongea, vitu ambavyo vinaishi, na vitu ambavyo vinapumua, vilevile vile ambavyo havipumui. Je, ni rahisi kwa vitu hivi vyote kupata uhusiano wa kutegemeana, wa kusaidiana na kuzuiana, wa kuingiliana? Kwa hakika kuna kanuni fulani ndani ya jambo hili. Inatatiza sana, siyo? Sio vigumu kwa Mungu, lakini kwa watu, inatatia sana kufanya utafiti. Ni neno rahisi

sana—uwiano. Hata hivyo, ikiwa watu wangelitafiti, ikiwa watu wangehitaji kutengeneza uwiano, basi hata kama wanataaluma wangukuwa wanalifanyia kazi—wanabiolojia wa kibinadamu, mamajusi, wanafizikia, wakemia na hata wanahistoria—matokeo ya mwisho ya utafiti huo yangukuwa ni yapi? Matokeo yake yasingekuwa chochote. Hii ni kwa sababu uumbaji wa Mungu wa vitu vyote ni wa ajabu sana na binadamu kamwe hataweza kufungua siri zake. Mungu alipoviumba vitu vyote, Alianzisha kanuni kati yao, Alianzisha njia tofautitofauti za kuendelea kuishi kwa ajili ya kuzuiana, kukamilishana, kuheshimiana, na riziki. Mbinu hizi mbalimbali zinatatiza sana; si rahisi au za kuelekea upande mmoja. Watu wanapotumia akili zao, maarifa ambayo wamepata, na matukio ambayo wameona kuthibitisha au kutafiti kanuni zinazoongoza udhibiti wa Mungu wa vitu vyote, vitu hivi ni vigumu sana kuvigundua, na pia ni vigumu sana kupata matokeo yoyote. Inaweza ikasemwa kwamba ni vigumu sana watu kupata matokeo yoyote. Ni vigumu sana kwa watu kupata matokeo yoyote; ni vigumu sana kwa watu kudumisha uwiano wao wanapoongoza vitu vyote vilivyoundwa na Mungu kwa kutegemea fikira na maarifa ya kibinadamu. Hii ni kwa sababu kama watu hawafahamu kanuni za kuendelea kuishi kwa vitu vyote, hawatajua jinsi ya kulinda aina hii ya uwiano. Kwa hiyo, ikiwa watu wanguweza kusimamia na kuongoza vitu vyote vya Mungu, kungekuwa na uwezekano mkubwa wa kuharibu uwiano. Mara tu utakapoharibiwa, mazingira yao kwa ajili ya kuendelea kuishi yanguweza kuharibiwa, na hiyo inapotokea, ingeweza kufuatiwa na mgogoro kwa ajili ya kuendelea kuishi kwao. Ingesababisha janga. Binadamu anapoishi katikati ya janga, nini kingeweza kutokea mbele yao? Yangukuwa ni matokeo ambayo ni vigumu kuyakisia, vigumu kuyabashiri.

Basi ni jinsi gani Mungu anaweka uwiano kwenye uhusiano kati ya vitu vyote? Kwanza, kuna baadhi ya maeneo duniani ambayo yamefunikwa na barafu na theluji kwa mwaka mzima, wakati katika baadhi ya maeneo, misimu yote minne ni kama msimu wa machipuo. Hutoweza kabisa kuona kipande cha barafu au chembe ya theluji—hakuna msimu wa baridi. Hii ni njia moja—ni kutokana na mtazamo mkubwa wa hali ya hewa. Njia ya pili ni hii: Safu ya milima iliyofunikwa na uoto uliostawi sana, ambapo aina zote za mimea inafunika ardhi; kuna malundo ya msitu na unapotentemba katikati yao huwezi hata kuona jua. Katika milima mingine nyasi hata hazioti—kuna safu na safu za milima yenye ukame, isiyokaliwa. Ukiangalia kwa nje, yote ni milima yenye mchanga uliorundikana. Kundi moja la milima limejaa uoto uliositawi, na kundi jingine halina hata nyasi. Hii ni aina ya pili. Katika aina ya tatu, unaweza kuona tabaka la mbuga lisilokuwa na kikomo, uwanda wa kijani unaopunga. Au unaweza kuona jangwa kadri jicho linavyoweza kuona; huoni kiumbe hai yeyote, wala chanzo chochote cha maji, ni sauti tu ya upepo pamoja na mchanga. Katika aina ya nne, sehemu moja imefunikwa na bahari, ambayo imeundwa na eneo kubwa la maji, wakati katika sehemu nyingine unahangaika sana kutafuta

chemchemi ya maji. Katika aina ya tano, katika nchi moja mvua ya manyunyu inanyesha mfululizo na ina ukungu na unyevunyevu, wakati kwenye nchi nyingine siku za jua kali ni za kawaida sana na hutaona hata tone moja la mvua. Katika aina ya sita, aina moja ya sehemu ni nchi tambarare ambapo hewa ni finyu sana na ni vigumu kwa binadamu kupumua, na katika aina nyingine ya eneo kuna kinamasi na nyanda za chini, ambayo yanatumika kama makazi ya aina mbalimbali ya ndege wahamao. Hizi ni aina tofautitofauti za tabia ya nchi, au tabia za nchi au mazingira ambayo yanaitikia mazingira tofautitofauti ya kijiografia. Hiyo ni sawa na kusema, Mungu anaweka uwiano kwenye mazingira ya msingi ya binadamu kwa ajili ya kuendelea kuishi kutoka katika mtazamo wa mazingira makubwa, kutoka katika tabia ya nchi kwenda katika mazingira ya kijiografia, kutoka katika vijenzi tofauti vya udongo kwenye kiwango cha vyanzo vya maji ili kupata uwiano kwenye hewa, halijoto na unyevunyevu wa mazingira ambamo watu wanaendelea kuishi. Kwa tofauti hizi za mazingira tofauti ya kijiografia, watu watakuwa na hewa imara na halijoto na unyevunyevu katika misimu tofautitofauti vitakuwa imara. Hii inawaruhusu watu kuendelea kuishi katika aina hiyo ya mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi siku zote. Kwanza, mazingira makubwa yanapaswa kuwekewa uwiano. Hii inafanyika kupitia kutumia kikamilifu maeneo mbalimbali ya kijiografia na muundo na vilevile muachano kati ya hali za nchi tofautitofauti kwa ajili ya kuzuiana ili kupata uwiano ambao Mungu anataka na ambao binadamu anahitaji. Hii ni kutokana na mtazamo wa mazingira makubwa.

Ukiangalia kwenye maelezo, kama vile uoto, inawezekanaje kuifanya hiyo ipate uwiano? Yaani, ni jinsi gani uoto unaweza kuruhusiwa kuendelea kuishi ndani ya mazingira yenye uwiano kwa ajili ya kuendelea kuishi? Ni kwa kusimamia urefu wa maisha, viwango vya ukuaji, na viwango vya kuzaliana vya aina mbalimbali za mimea ili kulinda mazingira yao kwa ajili ya kuendelea kuishi. Chukulia nyasi dogo kama mfano—wakati wa machipuo linachipua, wakati wa kiangazi linatoa maua, na wakati wa majira ya kupukutika majani linatoa matunda. Tunda linaanguka kwenye ardhi. Mwaka ujao, mbegu kutoka kwenye tunda inachipua na kukua kulingana na sheria zile zile. Urefu wa maisha ya nyasi ni mafupi sana. Kila mbegu inaanguka ardhini, inakuza mizizi na kuchipuka, inaweka maua na kuzaa matunda—hatua hii inatokea tu wakati wa machipuo, kiangazi na kupukutika, Aina zote za miti pia zina urefu wao wa maisha na vipindi tofauti kwa ajili ya kuchipua na kuzaa matunda. Baadhi ya miti hufa baada tu ya miaka 30 hadi 50—ina urefu wa maisha ya kuanzia miaka 30 hadi 50, lakini matunda yao huanguka ardhini, ambayo kisha hukuza mizizi na machipuko, maua na kuzaa tunda, na kuishi kwa miaka mingine 30 hadi 50. Hiki ndicho kiwango cha kujirudia kwake. Mti mzee unakufa na mti mdogo unakua—hii ndio maana siku zote unaona miti inaendelea kukua msituni. Lakini pia ina mzunguko wao mzuri na mchakato ama kuzaliwa na kufa. Baadhi ya miti inaweza kuishi kwa kipindi cha zaidi ya miaka elfu moja, na baadhi inaweza kuishi kwa hata miaka elfu tatu.

Haijalishi ni aina gani ya mmea au urefu wao wa maisha ni mrefu kiasi gani, nikizungumza kwa ujumla, Mungu anasimamia uwiano wake kulingana na kipindi unachoishi, uwezo wake wa kuzaliana, kasi yake ya kuzaliana vilevile kiasi na kiwango chake cha kuzaliana. Hii inawaruhusu, kuanzia majani hadi miti, kuweza kuendelea kusitawi, kukua ndani ya mazingira ya kiikolojia yenye uwiano. Kwa hiyo unapoangalia msitu duniani, haijalishi kama ni miti au majani, unaendelea kujizalisha na kukua kulingana na sheria zake. Haihitaji msaada wa binadamu; haihitaji kazi yoyote ya ziada kutoka kwa binadamu. Ni kwa sababu tu wana aina hii ya uwiano ndipo wana uwezo wa kudumisha mazingira yao kwa ajili ya kuendelea kuishi. Ni kwa sababu tu wana mazingira yanayofaa kwa ajili ya kuendelea kuishi ndipo misitu hii, kanda hizi za mbuga zinaweza kuendelea kuishi duniani. Uwepo wao unalea kizazi baada ya kizazi cha watu vilevile kizazi baada ya kizazi cha aina zote za viumbe hai vyenye makazi misituni na kwenye kanda za mbuga—ndege na wanyama, wadudu, na aina zote za vijiumbe.

Mungu pia anadhibiti uwiano wa aina zote za wanyama. Anadhibiti vipi uwiano huu? Ni sawa na kwenye mimea—anasimamia uwiano wao na anaamua idadi yao kulingana na uwezo wao wa kuzaliana, ukubwa na kiwango cha kuzaliana kwao na wajibu wanaoufanya miongoni mwa wanyama. Kwa mfano, simba hula pundamilia, kwa hiyo ikiwa idadi ya simba ingezidi idadi ya pundamilia, hatima ya pundamilia ingekuwaje? Wangepotea kabisa. Na ikiwa kuzaliana kwa pundamilia kungekuwa kwa idadi ndogo kuliko idadi ya simba, hatima yao ingekuwaje? Vilevile wangepotea kabisa. Kwa hiyo, idadi ya pundamilia inapaswa kuwa kubwa kuliko idadi ya simba. Hii ni kwa sababu pundamilia hawaishi tu kwa ajili yao; wanaishi pia kwa ajili ya simba. Unaweza pia kusema kwamba kila pundamilia ni sehemu moja ya pundamilia, lakini pia ni chakula katika kinywa cha simba. Kasi ya simba ya kuzaliana haiwezi kamwe kuiacha ile ya pundamilia, kwa hiyo idadi yao haiwezi kuwa kubwa kuliko idadi ya pundamilia. Ni kwa njia hii tu ndipo chanzo cha chakula cha simba kinaweza kuhakikishwa. Na kwa hivyo, ingawa simba ni maadui wa asili wa pundamilia, watu mara kwa mara huwaona wakiwa wamepumzika kwa kustarehe katika eneo moja. Pundamilia hawatapungua idadi au kupotea kabisa kwa sababu simba wanawawinda na kuwala, na simba hawataongezeka idadi yao kwa sababu ya hadhi yao kama “mfalme.” Uwiano huu ni kitu ambacho Mungu alikianzisha zamani sana. Yaani, Mungu alianzisha sheria za uwiano kati ya wanyama wote ili kwamba waweze kupata uwiano, na hiki ni kitu ambacho watu mara nyingi huona. Je, simba ni adui pekee wa asili wa pundamilia? La, mamba pia hula pundamilia. Pundamilia anaonekana kuwa mnyama asiyekuwa na msaada kabisa. Hawana ukali kama wa simba, na wanapomkabili adui huyu wa kutisha, wanaweza kukimbia tu. Hawawezi hata kutoa upinzani. Wakati ambapo hawawezi kumshinda mbio simba, wanaweza kujiruhusu tu waliwe naye. Hii inaweza kuonekana mara kwa mara katika ulimwengu wa wanyama. Mnapata wazo gani mnapoona kitu cha namna hii? Je, unamhurumia pundamilia?

Je, unamchukia simba? Pundamilia wanaonekana wazuri sana. Lakini simba, siku zote wanawaangalia kwa tamaa. Na kwa upumbavu, pundamilia hawakimbii mbali sana. Wanawaangalia simba pale wakiwasubiri, kwa kawaida wakiwasubiri chini ya kivuli cha mti. Nani anajua ni wakati gani atawala. Wanajua hili mioyoni mwao, lakini hawatalihama eneo hilo. Hili ni jambo la ajabu. Jambo hili la ajabu linajumuisha majaliwa ya Mungu, kanuni Yake. Unamhurumia pundamilia lakini huna uwezo wa kumsaidia, na unahisi kwamba simba ni wa kuchukiwa lakini huwezi ukamwepuka. Pundamilia ni chakula ambacho Mungu amekiandaa kwa ajili ya simba, lakini haijalishi ni kwa namna gani simba wanawala, pundamilia hawatamalizwa. Idadi ya watoto ambao simba wanazaa ni ndogo sana, na wanazaa polepole sana, kwa hiyo haijalishi ni pundamilia ngapi wanakula, idadi zao haziwezi kuzidi za pundamilia. Hii ni aina ya uwiano.

Lengo la Mungu ni lipi katika kudumisha aina hii ya uwiano? Hii inahusiana na mazingira ya watu kwa ajili ya kuendelea kuishi vilevile kuendelea kuishi kwa binadamu. Ikiwa pundamilia au mawindo mengine ya simba—paa au wanyama wengineo—watazaliana taratibu sana na idadi ya simba ikaongezeka haraka, ni aina gani ya hatari ambayo binadamu wangepata? Simba kuyala mawindo yao ni tukio la kawaida, lakini simba kumla mtu ni janga. Janga hili sio kitu ambacho kilipangwa kabla na Mungu, halipo ndani ya sheria Yake, wala kile ambacho amekileta kwa ajili ya binadamu. Badala yake, ni kile ambacho watu wamejiletea wenyewe. Kwa hiyo kama Mungu aonavyo, uwiano kati ya vitu vyote ni muhimu kwa ajili ya binadamu kuendelea kuishi. Iwe ni mimea au wanyama hawawezi kupoteza uwiano wao sahihi. Mimea, wanyama, milima, na maziwa—Mungu amewaandalia binadamu mazingira ya kawaida ya kiikolojia. Hadi pale tu ambapo watu watakuwa na aina hii ya mazingira ya kiikolojia—yenye uwiano—ndipo kuendelea kuishi kwao kutakuwa salama. Ikiwa miti au nyasi ingekuwa na uwezo mdogo wa kuzalisha au kasi yake ya uzalishaji ingekuwa ya taratibu sana, je, udongo ungepoteza unyevunyevu wake? Ikiwa udongo ungepoteza unyevunyevu wake, je, bado ungekuwa na afya? Ikiwa udongo ungepoteza uoto wake na unyevunyevu wake, ungemomonyoka haraka sana, na mchanga ungetokea badala yake. Wakati udongo ulipoharibika, mazingira ya watu kwa ajili ya kuendelea kuishi pia yangeharibika. Pamoja na uharibifu huu majanga yangeweza kutokea. Bila aina hii ya uwiano wa kiikolojia, bila aina hii ya mazingira ya kiikolojia, watu wangeendelea kuathirika na majanga kwa sababu ya kukosa uwiano baina ya vitu hivi vyote. Kwa mfano, wakati kunapokuwa na kukosekana kwa uwiano wa kimazingira hadi kusababisha uharibifu wa mazingira ya ikolojia ya vyura, wote wanakusanyika pamoja, idadi yao inaongezeka haraka sana na watu hata wanaona idadi kubwa ya vyura wanapita mtaani mijini, na idadi kubwa ya vyura barabarani. Ikiwa idadi kubwa ya vyura ingechukua sehemu kubwa ya mazingira ya watu kwa ajili ya kuendelea kuishi, hiyo ingeitwaje? Janga. Kwa nini liitwe janga? Wanyama hawa

wadogo ambao wana manufaa kwa binadamu wana faida kwa watu wanapobaki katika eneo ambalo linafaa kwao; wanadumisha uwiano wa mazingira ya watu kwa ajili ya kuendelea kuishi. Mara tu wanapokuwa janga, wataathiri mpangilio wa maisha ya watu. Vitu vyote na vipengele vyote ambavyo chura wanavileta vinaweza kuathiri ubora wa maisha ya watu. Hata ogani zao za kimwili zinaweza kushambuliwa—hii ni moja ya aina ya majanga. Aina nyingine ya janga, ambalo ni kitu ambacho binadamu wamepitia mara kwa mara—ni kutokea kwa idadi kubwa ya nzige. Hili si janga? Hili ni janga la kutisha. Haijalishi binadamu wana uwezo kiasi gani—watu wanaweza kutengeneza ndege, mizinga, na mabomu ya atomiki—lakini pale ambapo nzige wanawavamia binadamu, wanakuwa na suluhisho gani? Je, wanaweza kuwashambulia kwa mizinga? Je, wanaweza kuwafyatulia risasi kwa bunduki? Hawawezi. Basi wanaweza kuwanyunyizia dawa ya kuua wadudu ili kuwafukuza? Hiyo si rahisi pia. Hao nzige wadogo wanakuja kufanya nini? Wao haswa hula mimea na nafaka. Popote pale nzige wanapokwenda, mazao yanafutiliwa mbali kabisa. Kwa hivyo, chini ya uvamizi wa nzige, kufumba na kufumbua, chakula cha mwaka mmoja ambacho wakulima wanakitegemea kinaweza kuliwa kabisa na nzige. Kwa binadamu, ujio wa nzige sio tu kero—ni janga. Kutokea kwa nzige wengi ni aina ya janga, sasa vipi kuhusu panya? Ikiwa hakuna ndege wowote mbua wa kula panya, watazaliana haraka sana, haraka kuliko unavyoweza kufikiri. Na ikiwa kuenea kwa panya hakutadhibitiwa, je, binadamu wanaweza kuishi maisha mazuri?. Kwa hivyo ni kitu gani ambacho binadamu wangekabiliana nacho? (Tauni.) Tauni tu? Panya watatafuna kila kitu. Watatafuna hata mbao. Ikiwa kuna panya wawili tu katika nyumba, kila mtu kwenye nyumba yote atachukizwa. Wakati mwingine wanaiba mafuta na kula, wakati mwingine wanakula nafaka. Na vitu ambavyo hawali wanavitafuna tu na kuvivuruga kabisa. Wanatafuna nguo, viatu, fanicha—wanatafuna kila kitu. Wakati mwingine watapanda kwenye kabati la vyombo—je, vyombo hivyo bado vinaweza kutumiwa baada ya kukanyagwa na panya? Hata kama utavisafisha hutahisi una amani, kwa hiyo unavitupa tu nje. Hii ndiyo shida ambayo panya wanawapatia watu. Ni panya wadogo tu, lakini watu hawana namna ya kushughulika nao. Wamefanyiwa hata udhalimu na hao panya. Hakuna haja ya kuzungumzia kundi lote la panya—panya wawili tu wanatosha kufanya uharibifu. Kama wangukuwa janga, madhara yake hayawezi kufikirika. Na ikiwa mchwa wadogo wangukuwa janga, yale madhara ambayo wangufanya kwa binadamu pia yasingeweza kupuuzwa. Mchwa wanaweza kusababisha madhara kwa nyumba hadi zianguke. Uwezo wao haufai kupuuzwa. Halitakuwa jambo la kuogofya ikiwa aina tofauti za ndege wangesababisha janga? (Ndiyo.) Kusema vingine, haijalishi wao ni aina gani ya wanyama au viumbe hai, mara tu watakapopoteza uwiano wao, watakua, kuzaliana, na kuishi ndani ya mawanda yasiyokuwa ya kawaida, mawanda yasiyofuata kanuni. Hiyo ingeweza kuleta madhara yasiyoweza kufikirika kwa binadamu. Hiyo isingeweza kuathiri kuendelea kuishi na maisha ya watu tu, bali pia ingelea janga kwa binadamu, hata kufikia hatua ambapo watu watapatwa na maangamizo, watapatwa na

hatma ya kufa.

Mungu alipoumba vitu vyote, alitumia aina zote za mbinu na njia za kuziwekea uwiano, kuweka uwiano katika mazingira ya kuishi kwa ajili ya milima na maziwa, kuweka uwiano katika mazingira ya kuishi kwa ajili ya mimea na aina zote za wanyama, ndege, wadudu—lengo Lake lilikuwa ni kuruhusu aina zote za viumbe hai kuishi na kuongezeka ndani ya sheria ambazo alikuwa Amezianzisha. Hakuna hata kimoja katika viumbe wote kinachoweza kwenda nje ya sheria, na sheria haziwezi kuvunjwa. Ni ndani ya aina hii tu ya mazingira ya msingi ndipo binadamu wanaweza kuendelea kuishi kwa usalama na kuongezeka, kizazi baada ya kizazi. Ikiwa kiumbe yeyote anakwenda zaidi ya ukubwa au mawanda yaliyoanzishwa na Mungu, au ikiwa anazidi kiwango cha ukuaji, marudio, au idadi chini ya utawala Wake, mazingira ya binadamu kwa ajili ya kuendelea kuishi yangepata uharibifu wa viwango vinavyotofautiana. Na wakati uo huo, kuendelea kuishi kwa binadamu kungetishiwa. Ikiwa aina moja ya kiumbe hai ni kubwa sana kwa idadi, itawanyang'anya watu chakula chao, kuharibu vyanzo vya maji ya watu, na kuharibu makazi yao. Kwa njia hiyo, kuzaliana kwa binadamu au hali ya kuendelea kuishi ingeathiriwa mara moja. Kwa mfano, maji ni muhimu sana kwa vitu vyote. Ikiwa kuna idadi kubwa sana ya panya, siafu, nzige, na vyura, au wanyama wengine wa kila aina, watakunywa maji zaidi. Kadiri kiwango cha maji wanachokunywa kinaongezeka, ndani ya mawanda haya yasiyobadilika ya vyanzo vya maji ya kunywa na maeneo ya majimaji, maji ya kunywa ya watu na vyanzo vya maji vitapungua, na watapungukiwa maji. Ikiwa maji ya kunywa ya watu yataharibiwa, kuchafuliwa au kukatwa kwa sababu aina zote za wanyama zimeongezeka kwa idadi, chini ya aina hiyo ya mazingira katili kwa ajili ya kuendelea kuishi, kuendelea kuishi kwa binadamu hakika kutakuwa kumetishiwa vikali. Ikiwa kuna aina moja au aina kadhaa za viumbe hai ambavyo vinazidi idadi yao inayofaa, hewa, halijoto, unyevunyevu, na hata vijenzi vya hewa ndani ya eneo la binadamu kwa ajili ya kuendelea kuishi litakuwa na sumu na kuharibiwa kwa viwango vinavyotofautiana. Hali kadhalika, chini ya mazingira haya, kuendelea kuishi kwa binadamu na hatma bado vitakuwa chini ya tishio la aina hiyo ya mazingira. Kwa hiyo, ikiwa watu watapoteza uwiano huu, hewa wanayovuta itaharibiwa, maji wanayokunywa yatachafuliwa, na halijoto ambayo wanahitaji pia itabadilika, itaathiriwa kwa viwango tofautitofauti. Ikiwa hiyo itatokea, mazingira kwa ajili ya kuendelea kuishi ambayo kiasili ni ya wanadamu yataandamwa na madhara na changamoto kubwa. Chini ya aina hii ya mazingira ambapo mazingira ya msingi ya binadamu kwa ajili ya kuendelea kuishi yameharibiwa, hatma na matarajio ya binadamu yatakuwa ni nini? Ni tatizo kubwa sana! Kwa sababu Mungu anajua vitu vyote ni nini kwa binadamu, wajibu wa kila aina ya kitu Alichokiumba, aina gani ya athari kinacho kwa watu, na faida kubwa kiasi gani kinaleta kwa binadamu—katika moyo wa Mungu kuna mpango kwa ajili ya haya yote na Anasimamia kila kipengele cha vitu vyote alivyoviumba, kwa hiyo kwa

binadamu, kila kitu Anachofanya ni muhimu sana—vyote ni lazima. Kwa hiyo wakati unaona baadhi ya matukio ya kiikolojia miongoni mwa vitu vyote, au baadhi ya sheria za asili miongoni mwa vitu vyote, hutashuku tena ulazima wa kila kitu ambacho kiliumbwa na Mungu. Hutatumia tena maneno ya kijinga kufanya hukumu zisizokuwa na msingi juu ya mipangilio ya Mungu juu ya vitu vyote na njia zake mbalimbali za kuwakimu binadamu. Pia hutafanya mahitimisho yasiyokuwa na msingi juu ya sheria za Mungu kwa ajili ya vitu vyote ambavyo Aliviumba. Je, hii haiko hivyo?

Je, haya yote tuliyoyazungumza ni nini? Yafikirie. Mungu ana nia Yake katika kila kitu anachofanya. Ingawa binadamu hawawezi kuona nia hiyo, siku zote inahusiana na kuendelea kuishi kwa binadamu. Inahusiana bila kutenganishwa nayo—ni ya lazima. Hii ni kwa sababu Mungu hajawahi kufanya kitu ambacho hakina manufaa. Kwa kila kitu ambacho Anafanya, mpango Wake upo ndani ya nadharia na kanuni zake, ambazo zinajumuisha hekima Yake. Lengo na nia ya mpango huo ni kwa ajili ya ulinzi wa binadamu, kumsaidia binadamu kuzuia janga, uvamizi wa kiumbe chochote hai, na aina yoyote ya madhara kwa binadamu yasababishwayo na vitu vyote. Kwa hiyo kutokana na matendo ya Mungu ambayo tumeyaona kutoka katika mada hii ambayo tunaijadili, tungeweza kusema kwamba Mungu anawakimu binadamu kwa njia nyingine? Je, tungeweza kusema kwamba Mungu anawalisha na kuwachunga binadamu kwa njia hii? (Ndiyo.) Je, kuna uhusiano mkubwa kati ya mada hii na anwani ya ushirika wetu, “Mungu ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote”? (Ndiyo.) Kuna uhusiano mkubwa, na mada hii ni kipengele kimoja chake. Kabla ya kuzungumza kuhusu mada hizi, watu walikuwa tu na fikra zisizo dhahiri juu ya Mungu, Mungu Mwenyewe na matendo Yake—hawakuwa na uelewa wa kweli juu ya vitu hivi. Hata hivyo, watu wanapoambiwa kuhusu matendo Yake na vitu ambavyo Amefanya, wanaweza kuelewa na kufahamu kanuni za kile ambacho Mungu anafanya na wanaweza kupata kuzielewa na kuzikaribia—hivyo sivyo ilivyo? Ingawa katika moyo wa Mungu, nadharia Zake, kanuni Zake, na Sheria Zake zinatatiza sana Anapokuwa anafanya kitu chochote, Alipotengeneza vitu vyote, na Anapotawala vitu vyote, ikiwa kitu kimoja kimechukuliwa kushiriki na nyinyi katika ushirika, je, hamtaweza kuelewa mioyoni mwenu kwamba haya ni matendo ya Mungu, na yapo thabiti sana? (Ndiyo.) Basi ni kwa jinsi gani uelewa wenu wa sasa juu ya Mungu ni tofauti na ulivyokuwa kabla? Ni tofauti kwa asili yake. Mlichokielewa kabla kilikuwa tupu, kisicho dhahiri sana, na kila mnachokielewa sasa kinajumuisha kiasi kikubwa cha ushahidi thabiti kushikilia matendo ya Mungu, kulinganisha na kile Mungu anacho na alichoko. Kwa hiyo, yote ambayo nimeyasema ni nyenzo nzuri sana kwa ajili ya uelewa wa Mungu.

Hayo ndiyo yote katika mkutano wa leo. Kwaheri! Kuwa na jioni njema! (Kwa heri, Mungu!)

Februari 9, 2014

Mungu Mwenyewe, Yule wa Kipekee X

Mungu ni Chanzo cha Uhai kwa Vitu Vyote (IV)

Leo, tunafanya ushirika juu ya mada maalum. Kwa kila muumini, kuna vitu viwili vikuu tu ambavyo anapaswa kujua, kuvipitia na kuvielewa—na vitu hivi viwili ni vipi? Cha kwanza ni kuingia binafsi kwa watu katika maisha, na cha pili kinahusu kumjua Mungu. Mnadhani mambo ambayo tumekuwa tukiyafanyia ushirika hivi karibuni kuhusu kumjua Mungu yanawezekana? Ni haki kusema kuwa ni nje ya uwezo wa watu wengi. Mwaweza kukosa kusadiki maneno haya. Kwa nini Ninasema hili? Kwa sababu mlipokuwa mkisikiliza Niliyokuwa nikisema awali, haijalishi Niliyasema vipi, au ni kwa maneno gani, moja kwa moja na kinadharia mlikuwa mnatambua Nilichokuwa nikisema, lakini tatizo lenu kubwa ni kwamba, hamkuelewa ni kwa nini Niliyasema mambo haya, ni kwa nini nilizizungumzia hizi mada. Hiki ndicho kiini cha hili suala. Na kwa hiyo, japo kusikia kwenu haya mambo kuliongeza na kuimarisha uelewa wenu kuhusu Mungu na matendo Yake, bado mnapata ugumu kumjua Mungu. Baada ya kusikia Nilichokisema, wengi wenu hawaelewi ni kwa nini Nilisema hili, na lina uhusiano gani na kumjua Mungu. Sababu ya nyinyi kutoweza kuelewa uhusiano wake na kumjua Mungu ni uzoefu wenu wa kimaisha ni wa juujuu sana. Ikiwa ufahamu na uzoefu wa watu kuhusu maneno ya Mungu utabaki kuwa wa juujuu, basi ufahamu wao mkubwa kumhusu Mungu utakuwa si yakini na wa kidhahania; wote utakuwa wa jumla, wa kimafundisho, na wa kinadharia. Kinadharia, yanaonekana au kusikika kuwa na mantiki na razini, ila ufahamu kuhusu Mungu utokao vinywani mwa watu ni mtupu. Na mbona Ninasema kuwa ni mtupu? Kwa sababu, kwa hakika, moyoni mwako hauko wazi kama maneno kuhusu kumjua Mungu yatokayo kinywani mwako ni sawa au la, ikiwa ni sahihi au la. Hivyo basi, japo watu wengi wamesikia taarifa na mada nyingi kuhusu kumjua Mungu, ufahamu wao kuhusu Mungu haujatoka nje ya nadharia na zaidi ya kanuni ambayo ni sio wazi na dhahania. Jinsi gani, basi, hili tatizo linaweza kusuluhishwa vipi? Je, mmewahi kuliwazia hilo? Ikiwa watu hawautafuti ukweli, wanaweza kuwa na uhalisi? Ikiwa watu hawautafuti ukweli, basi bila shaka hawana uhalisi, na hivyo, kwa hakika hawana ufahamu au uzoefu wa maneno ya Mungu. Je, yawezekana wasioyafahamu maneno ya Mungu wamfahamu Mungu? Hawawezi Kabisa. Haya mawili yameshikamana. Hivyo, watu wengi husema, “Kumjua Mungu kwawezaje kuwa kugumu hivi? Ninapozungumzia kujijua mimi mwenyewe, naweza kuzungumza kwa saa nyingi, ila inapofika kumjua Mungu nakoswa maneno. Hata ninapoweza kusema machache, ni kwa kushurutishwa, yanakosa uchangamfu—hata yanasikika ya kufedhehesha ninapojisikia nikiyasema.” Hiki ndicho chanzo. Ukihisi kwamba kumjua Mungu ni kugumu sana, kwamba kunakuchosha, kwamba huna la

kuzungumzia—huna chochote cha kufanya ushirika na kuwapa wengine, na kujipa wewe mwenyewe—basi hili linathibitisha kwamba hujayapitia maneno ya Mungu. Maneno ya Mungu ni nini? Je, maneno ya Mungu sio maonyesho ya kile Mungu anacho na alichio? Ikiwa hujapitia uzoefu wa maneno ya Mungu, unaweza kuwa na ufahamu wowote kuhusu anacho na alichio. Kwa hakika siyo. Vitu hivi vyote vimeshikamana. Ikiwa huna uzoefu wa maneno ya Mungu, basi huwezi kuelewa mapenzi ya Mungu, na hutajua tabia Yake ni nini, Anachokipenda, Anachokichukia, mahitaji Yake kwa mwanadamu ni yapi, mtazamo Wake kwa walio wazuri, na kwa wale walio waovu ni upi—kwa hakika haya yote yatakuwa tata na yenye mashaka kwako. Ikiwa mnamwamini Mungu katikati ya haya mashaka, basi wakati unapodai kuwa miongoni mwa wale wanaoufuatilia ukweli na kumfuata Mungu, je, haya maneno yana uhalisi? Hayana! Hivyo tuendeleo kufanya ushirika kuhusu kumjua Mungu.

Nyinyi nyote mna shauku ya kuisikia mada tutakayoifanyia ushirika, sivyo? Mada tutakayowasiliana kwa karibu leo pia inahusiana na mada ya “Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote” ambayo tumekuwa tukizungumzia hivi karibuni. Tumeongea mengi kuhusu jinsi “Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote,” kutumia njia na mitazamo mbalimbali kuwaarifu watu jinsi Mungu anatawala juu ya vitu vyote, ni kwa njia gani Anavitawala vitu vyote, na ni kwa kanuni gani anavisimamia vitu vyote, ili kwamba viweze kuishi katika hii sayari Aliyomba Mungu. Tulizungumza pia mengi kuhusu jinsi ambavyo Mungu anamkimu mwanadamu: ni kwa njia gani Mungu anamkimu mwanadamu, ni mazingira ya kuishi ya aina gani Mungu anampa mwanadamu, na ni kwa njia zipi na kuanzia wapi Anampa mwanadamu mazingira thabiti ya kuishi. Japo Sikuzungumzia moja kwa moja uhusiano baina ya utawala wa Mungu juu ya vitu vyote, uendeshaji Wake wa vitu vyote na usimamizi Wake, kwa njia isiyokuwa ya moja kwa moja Nilisema ni kwa nini Anaviendesha vitu vyote namna hii, na ni kwa nini Anamkimu na kumlisha mwanadamu namna hii—yote ambayo yanahusu usimamizi wa Mungu. Maudhui tuliyoyazungumzia yalikuwa mengi na mapana—kuanzia mazingira makubwa hadi vitu vidogo zaidi kama mahitaji na lishe ya msingi ya wanadamu; kuanzia jinsi Mungu anaviongoza vitu vyote na kuvifanya vitende kazi kwa utaratibu, hadi kwenye mazingira ya kuishi sahihi na ya kufaa Aliyoyaumba kwa ajili ya watu wa kila jamii, na kadhalika. Haya maudhui mapana yanahusu jinsi mwanadamu anaishi katika mwili. Hivi ni kusema, yote yanahusiana na vitu katika ulimwengu halisi vinavyoonekana kwa macho ya kawaida, na ambavyo mwanadamu anaweza kuvihisi, kwa mfano, milima, mito, bahari, tambarare... Hivi vyote ni vitu vinavyoweza kuonekana na kuguswa. Nizungumzapo kuhusu hewa na halijoto, mnaweza kutumia pumzi zenu kuhisi moja kwa moja uwepo wa hewa, na miili yenu kuhisi kama halijoto iko juu au chini. Miti, nyasi, na ndege na wanyama porini, vitu vinavyopaa angani, na kutembea ardhini, na wanyama wadogo mbalimbali watokezao kutoka matunduni, vyote vinaweza kuonekana kwa wanadamu

kwa macho yao wenyewe na kusikika kwa masikio yao wenyewe. Japo mawanda ya vitu kama hivyo ni mapana, miongoni mwa vitu vyote vinawakilisha tu ulimwengu halisi. Vitu yakinifu ni vitu ambavyo watu wanaweza kuviona na kuvihisi, yaani, ukivigusa, utavihisi, na macho yako yakiviona, ubongo wako utakupatia umbo, picha. Ni vitu ambavyo ni halisi na kweli; kwako si dhahania, bali vina umbo; vinaweza kuwa mraba, au duara, au virefu au vifupi; na kila kimoja kinakupa taswira tofauti. Vitu hivi vyote vinawakilisha sehemu ile yakinifu ya vitu vyote. Na hivi, “vitu vyote” katika “utawala wa Mungu juu ya vitu vyote” vinajumuisha nini kwa Mungu? Havijumuishi tu vitu ambavyo watu wanaweza kuona na kugusa, bali, vilevile, visivyoonkana na visivyoshikika. Hii ni mojawapo ya maana za kweli za utawala wa Mungu juu ya vitu vyote. Hata kama vitu hivi havionekani na havishikiki kwa watu, kwa Mungu, alimradi vinaweza kuonekana kwa jicho Lake na vipo ndani ya ukuu Wake, kwa hakika vipo. Hata kama, kwa mwanadamu, ni dhahania na visivyofikirika—na hata kama, aidha, havionekani na havishikiki—kwa Mungu kwa kweli na kwa uhalisi vipo. Huo ndio ulimwengu mwingine wa vitu vyote ambavyo Mungu anatawala, na ni sehemu nyingine ya mawanda mengine ambayo Anatawala. Hii ndiyo mada ambayo tutaifanyia ushirika leo—jinsi Mungu anatawala na kuuongoza ulimwengu wa kiroho. Kwa kuwa mada hii inagusia jinsi Mungu anatawala na kusimamia vitu vyote, inahusiana na ulimwengu ulio nje ya ulimwengu yakinifu—ulimwengu wa kiroho—na kwa hivyo ni muhimu sana kwetu kuuelewa. Ni baada tu ya ushirika huu umetolewa na ni wakati tu watu wameuelewa ndipo wataweza kuelewa kwa hakika maana ya kweli ya maneno “Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote.” Hii ndiyo maana tutazungumzia mada hii. Na shabaha ya mada hii ni kukamilisha dhamira ya “Mungu anavitawala vitu vyote, na Mungu anavisimamia vitu vyote.” Pengine, mtakapoisikia mada hii, inaweza kuonekana ni ya ajabu na isiyoaminika kwenu—lakini bila kujali mnavyohisi, kwa kuwa ulimwengu wa kiroho ni sehemu moja ya vitu vinavyotawaliwa na Mungu, ni sharti mjifunze kitu kuhusu mada hii. Baada ya kujifunza, mtakuwa na ufahamu wa kina, uelewa na maarifa kuhusu maneno “Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote.”

Jinsi Mungu Anavyotawala na Kuongoza Ulimwengu wa Kiroho

Kwa ulimwengu yakinifu, watu wakikosa kuelewa vitu au jambo fulani, wanaweza kutafuta taarifa mwafaka, vinginevyo wanaweza kutumia njia mbalimbali kubaini asili ya habari kuvihusu. Lakini inapokuja kwa ulimwengu huu mwingine ambao tunauzungumzia leo—ulimwengu wa kiroho ulio nje ya ulimwengu yakinifu—watu hawana hasa mbinu au njia za kujifunzia chochote kuuhusu. Mbona Ninasema hivi? Kwa sababu, katika ulimwengu wa mwanadamu, kila kitu cha ulimwengu yakinifu hakijitengi na uwepo wa kimwili wa mwanadamu, na kwa sababu watu wanahisi kwamba kila kitu katika ulimwengu yakinifu hakitenganishwi na maisha yao ya kimwili na uhai wao wa kimwili, watu wengi wanafahamu tu

kuhusu, au kuona, vitu yakinifu mbele ya macho yao, vitu vinavyoonekana kwao. Bali inapokuja katika ulimwengu wa kiroho—yaani, kila kilicho cha ule ulimwengu mwingine—ni haki kusema kuwa watu wengi hawaamini. Kwa sababu watu hawawezi kuuona, wanaamini kuwa hakuna haja ya kuelewa au kujua kitu chochote kuuhusu, sembuse jinsi ulimwengu wa kiroho ni ulimwengu tofauti kabisa na ulimwengu yakinifu na kutoka kwa mtazamo wa Mungu, uko wazi—ingawa kwa wanadamu, ni wa siri na umefungwa—kwa hivyo watu huona ikiwa vigumu sana kupata njia ya kuelewa vipengele mbalimbali vya ulimwengu huu. Vipengele tofauti ambavyo nitazungumzia kuhusu ulimwengu wa kiroho vinahusu utawala na ukuu wa Mungu tu. Sifichui miujiza, wala Siwaambii siri zozote mnazotaka kugundua, kwani hili linahusu ukuu wa Mungu, utawala wa Mungu, na riziki ya Mungu, na kwa hivyo Sitazungumzia tu sehemu ambayo ni muhimu nyinyi kuijua.

Kwanza, hebu Niwaulize swali: katika mawazo yenu, ulimwengu wa kiroho ni nini? Kuzungumza kwa ujumla, ni ulimwengu ulio nje ya ulimwengu yakinifu, ambao hauonekani na haushikiki na watu. Lakini kwa fikra zenu, ulimwengu wa kiroho unafaa uwe ulimwengu wa aina gani? Pengine, kwa sababu ya kutoweza kuuona, mnaweza kushindwa kuufikiria. Lakini mtakaposikia hadithi kuuhusu, bado mtafikiri, hamtaweza kujizuia nyinyi wenyewe. Na kwa nini Ninasema hili? Kuna kitu kinachowatokea watu wengi wanapokuwa wachanga: mtu akiwasimulia hadithi ya kuogofya—juu ya mazimwi, na roho—wanaogopeshwa kabisa. Na kwa nini wanaogopeshwa? Ni kwa kuwa wanavifikiria vitu hivyo; hata japo hawawezi kuviona, wanahisi kuwa vipo kila pembe ya chumba chao, vimejificha sehemu fulani, au sehemu fulani yenye giza, na wanaogopa sana kiasi kwamba hawawezi kuthubutu kulala. Hasa wakati wa usiku, hawathubutu kuwa chumbani peke yao, au uani peke yao. Huo ndio ulimwengu wa kiroho wa fikra zenu, na ni ulimwengu ambao watu hudhani unaogofya. Kwa kweli, kila mtu ana fikra fulani, na kila mtu anaweza kuhisi kitu.

Hebu tuanze na ulimwengu wa kiroho. Ulimwengu wa kiroho ni nini? Hebu Niwape maelezo mafupi na rahisi. Ulimwengu wa kiroho ni sehemu muhimu, ambayo ni tofauti na ulimwengu yakinifu. Na mbona Ninasema kwamba ni muhimu? Tatalizungumzia hili kwa kina. Uwepo wa huu ulimwengu wa kiroho umeungana na ulimwengu yakinifu wa mwanadamu kwa njia isiyoweza kufumbulika. Una jukumu katika mzunguko wa uhai na mauti wa mwanadamu katika utawala wa Mungu juu ya vitu vyote; hili ndilo jukumu lake, na sababu mojawapo inayofanya uwepo wake kuwa muhimu. Kwa sababu ni mahali ambapo hapawezi kutambuliwa kwa milango mitano ya fahamu ya mwanadamu, hakuna anayeweza kubaini kwa hakika kuwepo au kutokuwepo kwake. Shughuli za ulimwengu wa kiroho zimeunganika kikamilifu na uwepo wa mwanadamu, na kwa sababu hiyo mpango wa maisha ya wanadamu pia unaathiriwa kwa kiwango kikubwa na ulimwengu wa kiroho. Je, hili linahusiana na ukuu wa Mungu?

Linahusiana. Nisemapo hili, unaelewa ni kwa nini Ninajadili mada hii; Kwa sababu inahusu ukuu wa Mungu, na utawala Wake. Katika ulimwengu kama huu—ulimwengu ambao hauonekani kwa watu—kila sheria yake ya peponi, amri na mfumo wake wa utawala ni wa juu zaidi kuliko sheria na mifumo ya nchi yoyote katika ulimwengu yakinifu, na hakuna kiumbe aishiye katika ulimwengu huu anaweza kuzivunja au kujitwalia bila haki. Je, hili linahusiana na ukuu na utawala wa Mungu? Katika ulimwengu huu kuna amri wazi za utawala, sheria wazi za mbinguni, na masharti wazi. Katika viwango tofauti na katika mawanda tofauti, wasimamizi huzingatia kikamilifu katika wajibu wao na kufuata sheria na masharti, kwa kuwa wanajua matokeo ya kukiuka sheria ya mbinguni ni yapi, wanafahamu wazi jinsi ambavyo Mungu anaadhibu maovu na kutuza mazuri, na kuhusu jinsi Anavyoviendesha vitu vyote, jinsi Anavyotawala vitu vyote, na zaidi, wanaona wazi ni jinsi gani Mungu anaendesha sheria za mbinguni na masharti Yake. Je, hizi ni tofauti na ulimwengu yakinifu unaokaliwa na wanadamu? Ni tofauti kwa kiasi kikubwa. Ni ulimwengu ambao ni tofauti kabisa na ulimwengu yakinifu. Kwa kuwa kuna sheria na masharti ya mbinguni, inahusu ukuu wa Mungu, utawala, aidha, tabia ya Mungu ya kile Anacho na alichio. Baada ya kusikia hili, hamhisi kwamba ni muhimu sana Mimi kuzungumzia hii mada? Hamtaki kujifunza siri zilizomo? (Ndiyo, tunataka.) Hiyo ndiyo dhana ya ulimwengu wa kiroho. Japo unapatikana sambamba na ulimwengu yakinifu, na wakati ule ule ukiwa chini ya utawala na ukuu wa Mungu, utawala na ukuu wa Mungu ya huu ulimwengu ni makali zaidi kuliko ulivyo ulimwengu yakinifu. Ikija katika maelezo, tunafaa tuanze na jinsi ulimwengu wa kiroho unawajibikia kazi ya mzunguko wa uhai na mauti ya mwanadamu, kwa kuwa kazi hii ni sehemu kuu ya viumbe wa ulimwengu wa kiroho.

Miongoni mwa wanadamu, Ninawaainisha watu katika aina tatu. Aina ya kwanza ni wasioamini, wale wasio na imani za kidini. Wanaitwa wasioamini. Wengi wa wasioamini wanaamini tu katika pesa, wanatafuta tu maslahi yao wenyewe, wana tamaa ya vitu, na wanaamini katika ulimwengu yakinifu, si katika mzunguko wa uhai na mauti au katika semi za miungu na mapepo. Ninawaainisha kama wasioamini na ni wa aina ya kwanza. Aina ya pili ni watu mbalimbali wenye imani tofauti na wasioamini. Miongoni mwa wanadamu, Ninawagawa hawa wenye imani katika aina kuu kadhaa: Ya kwanza ni Wayahudi, wa pili ni Wakatoliki, ya tatu ni Wakristo, ya nne ni Waislamu, na ya tano ni wafuasi wa Budha—kuna aina tano. Hizi ndizo aina mbalimbali za watu wenye imani. Aina ya tatu ni wale wanaomwamini Mungu, inayohusiana nanyi. Waumini kama hawa ni wale wanaomfuata Mungu leo. Hawa watu wamegawanyika katika aina mbili. Wateule wa Mungu na watendaji huduma. Hizi aina kuu zimebainishwa wazi. Basi sasa, akilini mwenu mnaweza kutofautisha wazi aina na madaraja ya binadamu, siyo? Ya kwanza ni wasioamini—nimesema wasioamini ni watu gani. Je, wale wanaomwamini Mtu Mzee aliye Angani wanahesabika kama wasioamini? Wengi wa wasioamini

wanamwamini yule Mzee aliye Angani; wanaamini kuwa upepo, mvua na radi, na kadhalika vyote vinadhibitiwa na huyu mtu ambaye wanamtegemea kwa upanzi wa mimea na uvunaji wa mazao—lakini wakati imani katika Mungu inatajwa, hawataki kumwamini. Je, hii yaweza kuitwa imani katika Mungu? Watu kama hao wanahesabiwa katika wasioamini. Mnaelewa hili, siyo?—Msifahamu visivyo vikundi hivi. Aina ya pili ni watu wa imani. Aina ya tatu ni wale wanaomfuata Mungu leo. Na kwa nini Nimewagawa wanadamu wote katika aina hizi? (Kwa sababu aina kadhaa za watu wana vituo na hatima tofautitofauti.) Hicho ni kipengele kimoja. Kwa sababu, wakati haya matabaka na aina mbalimbali za watu wanarudi katika ulimwengu wa kiroho, kila mmoja atakuwa na sehemu tofauti ya kuenda, watapitia sheria ya mzunguko tofauti wa uhai na mauti na hii ndiyo sababu Nimewaainisha wanadamu katika hizi aina kuu.

1. Mzunguko wa Uhai na Mauti wa Wasioamini

Hebu tuanze na mzunguko wa uhai na mauti wa wasioamini. Baada ya watu kufa, wanachukuliwa na msimamizi kutoka ulimwengu wa kiroho. Na ni kitu gani chao kinachukuliwa? Sio miili yao, bali ni roho zao. Roho zao zikichukuliwa, wanawasili katika sehemu ambayo ni ofisi ya ulimwengu wa kiroho, sehemu ambayo hasa hupokea roho za watu ambao wamekufa. (Kumbuka: sehemu ya kwanza wanapokwenda baada ya mtu yeyote kufa ni pageni kwa roho.) Wanapofikishwa mahali hapa, afisa anafanya ukaguzi wa kwanza, akithibitisha majina yao, anwani, umri, na uzoefu wao wote. Kila kitu walichofanya walipokuwa hai kinanakiliwa kwenye kitabu na usahihi wake unahakikishwa. Baada ya kukaguliwa, matendo na mienendo ya mtu maishani mwake vinatumika kuamua ikiwa ataadhibiwa au ataendelea kupata mwili kama mwanadamu, ambayo ni hatua ya kwanza. Je, hii hatua ya kwanza inaogofya? Haiogopeshi sana, kwani kitu cha pekee kilichofanyika ni kwamba mtu amewasili katika mahali pa giza na pageni.

Katika hatua ya pili, ikiwa mtu huyu amefanya mambo mengi mabaya maishani mwake, kama ametenda vitendo vingi viovu, basi atapelekwa mahali pa adhabu ili kuadhibiwa. Hiyo ndiyo itakuwa mahali ambapo kwa hakika ni kwa ajili ya adhabu ya watu. Maelezo kuhusu jinsi watakavyoadhibiwa yanategemea dhambi ambazo wamezitenda, pia ni vitendo vingapi viovu walitenda kabla hawajafa—hili ni tukio la kwanza ambalo linatokea katika hatua hii ya pili. Kwa sababu ya mambo mabaya waliyoyafanya, na maovu waliyoyafanya kabla hawajafa, wapatapo mwili baada ya adhabu yao—wazaliwapo upya tena katika ulimwengu yakinifu—watu wengine wataendelea kuwa wanadamu, na wengine watakuwa wanyama. Yaani, baada ya mtu kurudi katika ulimwengu wa kiroho, wanaadhibiwa kwa sababu ya maovu waliyotenda; zaidi, kwa sababu ya mambo maovu waliyofanya, watakapozaliwa tena katika mwili mpya huenda hawawi wanadamu, ila watakuwa mnyama. Baadhi ya wanyama watakaokuwa ni ng’ombe, farasi,

nguruwe, na mbwa. Watu wengine wanaweza kuwa ndege kule angani, au bata au bata bukini.... Baada ya kupata mwili kama mnyama, wanapokufa wanarudi katika ulimwengu wa kiroho, na sawa na mara ya kwanza, kutegemea mienendo yao kabla hawajafa, ulimwengu wa kiroho utaamua kama wapate mwili kama mwanadamu au la. Watu wengi hutenda maovu mengi sana, dhambi zao ni nzito sana, na kwa hivyo wapatapo mwili wanakuwa wanyama mara saba hadi mara kumi na mbili. Mara saba hadi mara kumi na mbili—hilo linaogopesha? (Linaogopesha.) Ni nini kinawaogopesha? Mtu kuwa mnyama, hilo linaogopesha. Na kwa mwanadamu, ni kipi cha uchungu zaidi kuhusu kuwa mnyama? Kutokuwa na lugha, kuwa tu na mawazo sahili, kuweza tu kufanya vitu ambavyo wanyama hufanya na kula vitu ambavyo wanyama hula, na kuwa na fikira sahili na kuwa na viziada lugha vya mnyama, kutoweza kutembea wima, kutoweza kuwasiliana na wanadamu, na mienendo yoyote na vitendo vya wanadamu kutokuwa na uhusiano na wanyama. Yaani, miongoni mwa vitu vyote, kuwa mnyama kunakufanya kuwa chini zaidi ya viumbe hai wote, na ni kuchungu zaidi kuliko kuwa mwanadamu. Hiki ni kipengele kimoja cha adhabu ya ulimwengu wa kiroho kwa wale waliofanya maovu mengi na kutenda dhambi kubwa. Ukali wa adhabu utakavyokuwa, hili hubainishwa na aina ya mnyama ambaye mtu anakuwa. Kwa mfano, kuwa nguruwe ni bora kuliko kuwa mbwa? Je, nguruwe huishi vizuri au vibaya kuliko mbwa? Vibaya zaidi, siyo?. Watu wakiwa ng'ombe au farasi, je, wataishi vizuri zaidi au vibaya kuliko jinsi wangesishi kama nguruwe? (Vizuri zaidi.) Je, mtu atakuwa wa faraja zaidi kama mtu angezaliwa kama paka? Angekuwa mnyama sawa tu, na kuwa paka ingekuwa rahisi zaidi kuliko kuwa ng'ombe au farasi, kwa sababu paka huweza kuupitisha muda wao mwingi kulala. Kuwa ng'ombe au farasi ni kazi nzito. Hivyo basi, iwapo mtu atapata mwili na kuwa ng'ombe au farasi, wanapaswa kutia bidii—ambayo ni sawa na adhabu nzito. Kuwa mbwa kungekuwa ni afadhali kidogo kuliko kuja kuwa ng'ombe au farasi, kwa kuwa mbwa ana uhusiano wa karibu na bwana wake. Baadhi ya mbwa, baada ya kuwa kipenzi kwa miaka mingi, wanaweza kuelewa mengi ya yale bwana wao wanasema! Wakati mwingine na mahitaji yake na bwana anamtunza mbwa vyema, na mbwa anakula na kunywa vyema, na akiwa na maumivu anatumzwa zaidi. Je, mbwa basi hapati maisha ya furaha? Hivyo basi, kuwa mbwa ni bora kuliko kuwa ng'ombe au farasi. Katika hili, ukali wa adhabu ya mtu unaamua ni mara ngapi mtu hupata mwili kuwa mnyama, pia wa aina gani.

Kwa sababu walitenda dhambi nyingi sana walipokuwa hai, watu wengine wataadhibiwa kwa kupatiwa miili kama wanyama mara saba hadi kumi na mbili. Baada ya kuadhibiwa vya kutosha, wanaporudi katika ulimwengu wa kiroho wanapelekwa mahali pengine. Roho mbalimbali mahali hapa zimeadhibiwa tayari, na ni aina ya roho ambazo ziko tayari kupata mwili kama wanadamu. Mahali hapa panaziainisha roho katika makundi kulingana na aina ya familia watakamozaliwa, ni aina gani ya nafasi watashikilia baada ya kupata mwili, na kadhalika.

Kwa mfano, watu wengine watakuwa waimbaji wakija katika ulimwengu huu, na kwa hivyo wanawekwa miongoni mwa waimbaji; wengine watakuwa wafanyabiashara wakija katika ulimwengu huu, na kwa hivyo wanawekwa miongoni mwa wafanyabiashara; na ikiwa mtu atakuwa mtafiti wa kisayansi akiwa mwanadamu, basi anawekwa miongoni mwa watafiti wa kisayansi. Baada ya kuwekwa katika makundi, kila mmoja anatumwa kulingana na wakati tofauti na tarehe iliyowekwa, sawa tu na jinsi watu hutuma barua pepe siku hizi. Katika hili kutakuwa kumekamilika mzunguko mmoja wa uhai na mauti. Tangu siku mtu anapowasili katika ulimwengu wa kiroho hadi mwisho wa adhabu yake, ama hadi anapozaliwa upya kama mnyama mara nyingi na anajitayarisha kuzaliwa upya kama mwanadamu, huu ni mchakato mzima.

Na wale waliokamilisha adhabu yao, na hawajapata mwili kuwa wanyama, je, watapelekwa kwa haraka katika ulimwengu yakinifu kuwa wanadamu? Au watachukua muda gani ndipo waje miongoni mwa wanadamu? Hili linaweza kurudiwa mara ngapi? Kwa hili kuna mipaka ya wakati. Kila kitu kinachofanyika katika ulimwengu huu wa kiroho kinapitia mipaka ifaayo kwa wakati na sheria—ambayo, Nikiieleza kutumia tarakimu, mtaelewa. Kwa wapatao mwili baada ya muda mfupi, wakati wanapokufa kuzaliwa kwao upya kama wanadamu kutatayarishwa. Wakati mfupi zaidi ni siku tatu. Kwa watu wengine, ni miezi mitatu, kwa wengine ni miaka mitatu, kwa wengine ni miaka thelathini, kwa wengine ni miaka mia tatu, kwa wengine hata ni miaka elfu tatu, na kadhalika. Hivyo basi ni nini kinaweza kusemwa kuhusu hizi sheria za wakati, na vipimo vyake ni vipi? Vinalingana na ulimwengu yakinifu, ulimwengu wa mwanadamu unahitaji kutoka kwa roho, na nafasi itakayochukuliwa na hii roho duniani. Watu wakipata mwili kama wanadamu wa kawaida, wengi wao wanapewa mwili haraka sana, kwa sababu dunia ya wanadamu ina uhitaji mkubwa wa watu wa kawaida kama hao, na kwa hiyo siku tatu baadaye wanatumwa tena katika familia ambayo ni tofauti kabisa na ile waliyokuwa kabla hawajafa. Lakini wapo ambao wana nafasi maalum katika ulimwengu huu. “Maalum” inamaanisha kuwa hakuna uhitaji mkubwa wa hawa watu katika ulimwengu wa wanadamu; si watu wengi wanaohitajika kuishikilia nafasi hiyo, kwa hiyo basi inaweza kuwa miaka mia tatu kabla hawajapata mwili. Ambako ni kusema, hii roho itakuja mara moja tu katika kila miaka mia tatu, au hata mara moja kila baada ya miaka elfu tatu. Na ni kwa nini hivi? Ni kwa sababu kwa miaka mia tatu au miaka elfu tatu, nafasi hiyo haihitajiki katika dunia ya mwanadamu, na kwa hiyo wanatunzwa mahali fulani katika ulimwengu wa kiroho. Tazama Confucius, kwa mfano. Alikuwa na athari kubwa katika utamaduni wa jadi wa Uchina. Kuwasili kwake kulikuwa na athari kubwa kwenye utamaduni, elimu, desturi, na kufikiri kwa watu wa wakati ule. Lakini mtu kama huyu hahitajiki katika kila enzi, na kwa hiyo alilazimika kubaki katika ulimwengu wa kiroho, akisubiri huko kwa miaka mia tatu au miaka elfu tatu kabla ya kupata mwili. Kwa kuwa ulimwengu wa mwanadamu haukuhitaji mtu kama huyu, alilazimika kusubiri bila kufanya

chochote, kwa kuwa kulikuwa na nafasi chache sana kama yake, kulikuwa na machache ya yeye kufanya, na hivyo basi alitunzwa sehemu fulani katika ulimwengu wa kiroho kwa muda mrefu, bila kufanya chochote, na kutumwa wakati ambapo ulimwengu wa mwanadamu ulimhitaji. Hizo ndizo sheria za wakati za milki ya kiroho kuhusu haraka ambayo watu wengi wanapata miili. Iwe ni mtu wa kawaida au maalum, ulimwengu wa kiroho una sheria mwafaka na desturi sahihi kwa utayarishaji wa watu kuzaliwa katika mwili mpya, na hizi sheria na desturi zinatumiwa kutoka kwa Mungu, na haziamuliwi au kudhibitiwa na msimamizi yeyote au kiumbe chochote katika ulimwengu wa kiroho. Sasa mnaelewa, naam?

Kwa nafsi yoyote, kuzaliwa kwake katika mwili mpya, nafasi yake ni ipi katika haya maisha, atazaliwa katika familia gani, na maisha yake yatakuwaje vinahusiana kwa karibu na maisha yake ya zamani. Watu wa kila aina huja katika dunia ya wanadamu, na nafasi zao ni tofauti, kama zilivyo kazi wazifanyazo. Na hizi ni kazi gani? Watu wengine wanakuja kulipa deni: Ikiwa walikuwa na pesa nyingi za watu katika maisha yao ya awali, wanakuja kulipa deni. Katika maisha haya Wakati uleule, watu wengine, wamekuja kuchukua madeni yao: Walitapeliwa vitu vingi sana, na pesa nyingi sana katika maisha yao yaliyopita, na kwa hiyo, baada ya kuwasili katika ulimwengu wa kiroho, ulimwengu wa kiroho utawapa haki na kuwapa fursa ya kukusanya madeni yao katika maisha haya. Watu wengine wamekuja kulipa deni la shukrani: katika maisha yao yaliyopita—kabla hawajafa—mtu alikuwa mkarimu kwao, na katika maisha haya wamepatiwa fursa nzuri kupata mwili ili kwamba waweze kuzaliwa upya ili kulipa upya deni hili la shukrani. Wakati uleule, wengine wamezaliwa upya katika haya maisha ili kudai uhai. Na wanadai uhai wa nani? Uhai wa mtu aliyewaua katika maisha yao yaliyopita. Kwa ujumla, maisha ya sasa ya kila mtu yana uhusiano mkubwa na maisha yao yaliyopita, yameungana kwa njia isiyoachana. Yaani, maisha ya sasa ya kila mtu yanaathiriwa pakubwa na maisha yao yaliyopita. Kwa mfano, kabla ya kufariki, Zhang alimtapeli Li kiwango kikubwa cha pesa. Je, Zhang ana deni la Li? Kwa kuwa analo, ni kawaida kwamba Li anapaswa kuchukua deni lake kutoka kwa Zhang? Hivyo basi baada ya wao kufa, kuna deni kati yao ambalo linatakiwa kulipwa. Wakati wanapata mwili mpya na Zhang anakuwa mwanadamu, je, Li anapataje deni hili kutoka kwake? Mbinu moja ni kwamba Li anapata deni lake kwa kuzaliwa upya kama mwana wa Zhang, Zhang anapata pesa nyingi, na zinaliwa na Li. Haijalishi Zhang anapata pesa nyingi kiasi gani, mwana wa Li anazitumia ovyo. Haijalishi Zhang anapata kiasi gani cha pesa, katu hazitoshi, wakati uleule, mwanawe, kwa namna fulani daima anazitumia pesa za babake kupitia njia na mbinu mbalimbali. Zhang anachanganyikiwa: “Kwa nini mwanangu daima amekuwa kisirani? Mbona wana wa watu wengine ni wema sana? Ni kwa nini mwanangu hana lengo, ni kwa nini hana maana na hana uwezo wa kuchuma pesa zozote, kwa nini daima ninapaswa kumsaidia? Kwa kuwa ni lazima nimsaidie, nitamsaidia, ila kwa nini hata nimpe pesa

kiasi gani, daima anataka zaidi? Ni kwa nini asifanye kazi halali, lakini atafanya chochote—kuzurura, kula, kunywa, kuzini, na kucheza kamari? Nini kinaendelea?” Halafu Zhang anafikiria kidogo: “Inaweza kuwa ni kwa sababu nilikuwa na deni lake katika maisha ya zamani. Sawa basi, nitalilipa! Haya hayataisha hadi nilipe kikamilifu!” Inaweza kufika siku ambayo Li anafidia deni lake, na akiwa na umri wa miaka arobaini au hamsini, itafika siku ambayo atajitambua: “Sijafanya kitu kizuri hata kimoja katika hii nusu ya kwanza ya maisha yangu! Nimefuja pesa zote alizozipata baba—ninapaswa kuwa mtu mwema! Nitajikakamua: nitakuwa mtu ambaye ni mwaminifu, na anayeishi ipasavyo, na sitamletea babangu huzuni tena!” Kwa nini anafikiria hivi? Mbona anageuka kuwa mwema ghafla? Kuna sababu ya hili? Ni sababu gani? (Kwa sababu Li amepokea deni lake; Zhang amelipa deni lake.) Katika hili, kuna chanzo na matokeo. Kisa kilianza zamani sana, kabla hawa wawili hawajazaliwa, na hiki kisa cha maisha yao ya zamani kimeletwa katika maisha yao ya sasa, na hakuna anayeweza kumlaumu mwingine. Haijalishi Zhang alimfundisha nini mwanake, mwanake hakumsikiliza, na hakufanya kazi halali hata ya siku—lakini siku ambayo deni lilipwa, hapakuwa na haja ya kumfundisha; mwanake alielewa kiasili. Huu ni mfano rahisi. Kuna mifano mingine mingi kama huu? (Ndiyo.) Na unawafunza watu kitu gani? (Wanapaswa kuwa wema na hawapaswi kutenda maovu.) Kwamba hawapaswi kutenda maovu, na kutakuwa na adhabu kwa maovu yao! Wengi wa wasioamini, hutenda maovu mengi na utendaji maovu wao umekutwa na adhabu, sawa? Je, hii adhabu ni ya kinasibu? Kila linalokutwa na adhabu lina asili na sababu. Unadhani hakuna litakalotendeka baada ya kumlaghai mtu pesa? Unadhani baada ya kuwatapeli pesa zao hakutakuwa na matokeo kwako baada ya kuchukua pesa zao? Hilo halitawezekana, na kutakuwa na athari! Bila kujali yeye ni nani, au kama anaamini ama haamini kuwa kuna Mungu, kila mtu ni lazima atawajibikia mienendo yake na kubeba matokeo ya matendo yake. Kwa kurejelea huu mfano rahisi—Zhang kuadhibiwa, na Li kulipwa—je hii si haki? Watu wakifanya vitu kama hivyo, kuna aina hiyo ya matokeo. Haitenganishwi na utawala wa ulimwengu wa kiroho. Licha ya kuwa wasioamini, wale wasiomwamini Mungu, uwepo wao uko chini ya amri za peponi na sheria ambazo haziwezi kuepukika na yeyote na hakuna mtu anayeweza kuepuka ukweli huu.

Wale ambao hawana imani huamini kuwa kila kitu ambacho kinaweza kuonekana kipo, ilhali kila kitu kisichoonekana, au ambacho kiko mbali sana na watu, hakipo. Wanapenda kuamini kuwa hakuna “mzunguko wa uhai na mauti,” na hakuna “adhabu,” na kwa hiyo wanatenda dhambi na kufanya maovu bila majuto—ambayo baadaye wataadhibiwa kwayo, au watapata miili kama mnyama. Wengi wa watu mbalimbali miongoni mwa Wasioamini wanapatikana katika mzunguko huu. Ni kwa sababu hawajui kuwa ulimwengu wa kiroho ni mkali katika kuviendesha viumbe hai wote. Ikiwa unaamini au la, huu ukweli upo, na hakuna mtu hata mmoja au chombo chochote kinaweza kuepuka mawanda ya ambacho kinaonwa na

macho ya Mungu, na hakuna mtu hata mmoja au chombo kinachoweza kuepuka sheria na mipaka ya sheria za peponi na amri za Mungu. Na hivyo basi mfano huu rahisi unamwambia kila mtu kwamba haijalishi kama unamwamini au humwamini Mungu, haikubaliwi kutenda dhambi na kufanya maovu, na kuna matokeo. Wakati mtu aliyemlaghai mwingine pesa anaadhibiwa hivyo, hiyo adhabu ni ya haki. Mienendo inayoonekana ya kawaida kama hii inaadhibiwa na ulimwengu wa kiroho, inaadhibiwa na amri na sheria za mbinguni za Mungu, na vivyo hivyo uhalifu mkubwa na matendo maovu—ubakaji na unyang'anyi, ulaghai na udanganyifu, wizi na ujambazi, mauaji na uchomaji, na kadhalika—yanapitia adhabu za aina zenye ukali wa viwango mbalimbali. Na hizi adhabu zenye ukali wa viwango mbalimbali zinajumuisha nini? Baadhi yake zinatimia muda kufikisha kiwango cha ukali, na nyingine hufikiwa kwa mbinu mbalimbali, na nyingi hufikiwa kupitia mahali mtu aendapo akipata mwili. Kwa mfano, watu wengine wana maneno machafu. Kuwa na “maneno machafu” kunamaanisha nini? Kunamaanisha kuwaapiza wengine mara kwa mara, na kutumia lugha chafu, lugha inayowalaani watu wengine. Lugha yenye nia mbaya inaashiria nini? Inaashiria kuwa mtu ana roho mbaya. Lugha yenye nia mbaya inayowalaani watu wengine mara nyingi inatoka vinywani mwa watu kama hao, na lugha yenye nia mbaya kama hiyo mara nyingi inaandamana na matokeo makali. Baada ya hawa watu kufa na kupokea adhabu stahili, wanaweza kuzaliwa kama mabubu. Watu wengine ni wajanja sana wakiwa hai, mara kwa mara wanawatumia watu wengine kwa manufaa yao, njama zao huwa zimepangwa barabara, na wanafanya mengi yanayowadhuru wengine. Wakizaliwa upya, wanaweza kuwa wazimu au punguani. Watu wengine mara nyingi huwachungulia watu wengine wakiwa faraghani; macho yao huona mengi ambayo hawakutakiwa kuona, na hujua mengi ambayo hawakupaswa kujua, hivyo basi wazaliwapo upya, wanaweza kuwa vipofu. Watu wengine ni hodari sana wakiwa hai, wanapigana mara kwa mara, na kufanya mengi ambayo ni maovu, na kwa hiyo wanapozaliwa upya, wanaweza kuwa vilema au wakakosa mkono, vinginevyo wanaweza kuwa vibyongo, au wenye shingo iliyopinda, huenda wakatembea wakichechemea, au wakawa na mguu mmoja mfupi kuliko mwingine, na kadhalika. Katika hali hii, wanapewa adhabu mbalimbali kutegemea kiwango cha maovu waliyotenda walipokuwa hai. Mwasemaje, kuhusu ni kwa nini watu huwa na makengeza? Je, kuna watu wengi wa hivyo? Kuna wengi wao siku hizi. Watu wengine wana makengeza kwa sababu waliyatimia macho yao sana katika maisha yao yaliyopita, walifanya mambo mengi mabaya, na kwa hiyo wazaliwapo katika haya maisha macho yao hupata makengeza, na katika hali mbaya, hata huwa vipofu. Haya ni malipo! Watu wengine wanaelewana vizuri na wengine kabla hawajafa, wanafanya mambo mengi mazuri kwa wapendwa wao, marafiki, wenza, au watu wanaohusiana nao. Wanatoa hisani na matunzo kwa wengine, au kuwasaidia kifedha, wengine wanawaheshimu sana, na watu kama hao warudipo katika ulimwengu wa kiroho hawaadhibiwi. Kwa asiyeamini kukosa kuadhibiwa kwa njia yoyote inamaanisha alikuwa mtu mzuri sana. Badala ya kuamini katika uwepo wa

Mungu, wanaamini tu katika Mzee aliye Angani. Wanaamini tu kuwa kuna roho juu yao akitazama yote wafanyayo—hayo tu ndiyo wanaamini. Na matokeo ni kwamba wanakuwa na mwenendo mzuri zaidi. Hawa watu ni wenye huruma na wakarimu, na mwishowe wakirudi katika ulimwengu wa kiroho, ulimwengu wa kiroho utawapokea vizuri sana na watapata mwili na kuzaliwa upya mapema. Wanapozaliwa tena, watafikia katika familia za aina gani? Japo familia yake haitakuwa ya kitajiri, itakuwa tulivu, kutakuwa na maelewano miongoni mwa wanafamilia, watakuwa na siku mwanana, za kupendeza, kila mmoja atafurahia, na watakuwa na maisha mazuri. Naye atakapokuwa mtu mzima, atakuwa na familia kubwa na jamaa wengi, watoto wake watakuwa na vipawa na kufanikiwa, na familia yake watakuwa na bahati nzuri—na matokeo kama hayo yanahusiana kwa kiasi kikubwa na maisha ya zamani ya mtu. Yaani, mahali mtu huenda baada ya kufa na kupata mwili, wawe wanaume au wanawake, wito wao ni upi, watapitia nini maishani, vikwazo vyao, watapata baraka gani, watakutana na nani, ni nini kitawatokea—hakuna awezaye kulitabiri hili, kuliepuka, au kujificha kutokana nalo. Yaani, baada ya maisha yako kupangwa, kitakachokutokea, hata ujaribu namna gani kukikwepa, hata ukitumia mbinu gani kukiepuka, huna njia ya kuvuruga mkondo wa maisha uliopangiwa na Mungu katika ulimwengu wa kiroho. Kwani upatapo mwili, majaaliwa yako tayari huwa yameishapangwa, ikiwa yatakuwa mazuri au mabaya, kila mtu anapaswa kuyakubali yalivyo, na anapaswa kusonga mbele; hili ni jambo ambalo hakuna mtu aishiye katika maisha haya anaweza kuliepuka, na huu ndio uhalisia. Sawa, umeyaelewa haya yote, naam?

Baada ya kulielewa hili, mnaona kwamba Mungu ana uangalizi unaolipiza sana na mkali pamoja na utawala kwa mzunguko wa uhai na mauti wa wasioamini? Kwanza, Mungu ameweka sheria mbalimbali za mbinguni, amri, na mifumo katika milki ya kiroho, na baada ya kutangazwa kwa hizi sheria za mbinguni, amri na mifumo, ambazo zinatekelezwa kabisa, kama zilivyopangwa na Mungu, na viumbe wenye nyadhifa rasmi mbalimbali katika ulimwengu wa kiroho, na hakuna anayethubutu kuzikiuka. Na kwa hivyo, katika Mzunguko wa uhai na mauti wa wanadamu katika dunia ya mwanadamu, mtu awe amepata mwili kama mwanadamu au mnyama, kuna sheria kwa yote mawili. Kwa kuwa sheria hizi zinatoka kwa Mungu, hakuna anayethubutu kuzivunja, wala hakuna awezaye kuzivunja. Ni kwa sababu tu ya huo ukuu wa Mungu, na kwa sababu kuna sheria hizo, ndiyo ulimwengu yakinifu uonekanao kwa mwanadamu ni wa kawaida na wenye mpangilio; ni kwa sababu tu ya ukuu wa Mungu ndipo mwanadamu anaweza kuishi kwa amani pamoja na ulimwengu mwingine ambao hauonekani kabisa kwa mwanadamu, na kuweza kuishi nao kwa amani—vitu ambavyo vyote haviwezi kutenganishwa na mamlaka ya Mungu. Baada ya maisha ya mtu ya kimwili kufa, roho bado huwa na uhai, basi ni nini kingetendeka ikiwa roho ingekosa utawala wa Mungu? Roho ingezurura kila mahali, ikiingia kila sehemu, na hata kudhuru viumbe hai katika ulimwengu wa

wanadamu. Madhara hayo hayangekuwa tu kwa mwanadamu bali pia kwa mimea na wanyama—ila wa kwanza kudhuriwa wangekuwa watu. Kama hili lingetukia—roho kama hiyo ingekosa uendesaji, na kuwadhuru watu kwa hakika, na kufanya mambo maovu kwa hakika—basi pia kungekuwa na ushughulikiaji ufaao wa roho hii katika ulimwengu wa kiroho: Ikiwa mambo yangekuwa mabaya, roho haingeendelea kuwepo, ingeamizwa; ikiwezekana, ingewekwa mahali fulani halafu ipatiwe mwili. Yaani, utawala wa ulimwengu wa kiroho kwa roho mbalimbali umepangiliwa, na kutekelezwa kulingana na hatua na sheria. Ni kwa sababu tu ya utawala huo ndiyo ulimwengu yakinifu wa mwanadamu haujatumbukia kwenye machafuko, ndiyo mwanadamu wa ulimwengu wa kuonekana ana akili ya kawaida, urazini wa kawaida, na maisha ya kimwili yenye mpangilio. Ni baada tu ya mwanadamu kuwa na maisha ya kawaida ndiyo wale wanaoishi katika mwili wanaweza kuendelea kufanikiwa na kuzaana katika vizazi vyote.

Mnafikiri nini kuhusu maneno ambayo mmesikia hivi punde? Je, ni mageni kwenu? Na mnahisi nini baada ya Mimi kuwasiliana maneno haya leo? Licha ya kwamba ni mapya, mnahisi kitu kingine chochote? (Ni lazima watu wawe na tabia nzuri, na ninaona Mungu ni mkubwa na wa kuogopwa.) (Baada ya kusikia kuwasiliana kwa karibu kwa Mungu kuhusu jinsi Mungu hupanga hatima za aina mbalimbali za watu, kwa upande mmoja ninahisi kuwa tabia ya Mungu haikubali kosa lolote, na kwamba ninapaswa kumheshimu sana; na kwa upande mwingine, ninafahamu Mungu anapenda aina gani ya watu, na ni aina gani hapendi, kwa hivyo ninataka kuwa mmoja wa wale ambao Mungu anapenda.) Je, mnaona kwamba Mungu ni mwenye kanuni katika matendo Yake katika mambo haya? Anatenda kulingana na kanuni gani? (Anapanga hatima za watu kulingana na yote wanayoyafanya.) Hii inahusu hatima mbalimbali za wasioamini ambao tumezungumzia. Ikija kwa wasioamini, je, kanuni iongozayo matendo ya Mungu ni ile ya kutuza mazuri na kuadhibu mabaya? Kuna upekee wowote? (La.) Je, mnaona kwamba kuna kanuni katika matendo ya Mungu? Wasioamini kwa hakika hawamwamini Mungu, hawatii mipango ya Mungu, na hawafahamu ukuu wa Mungu, na hawamtambui Mungu hata kidogo. Zito zaidi, wanamkufuru Mungu, na kumlaani, na ni mahasimu wa wale wanaomwamini Mungu. Japo watu hawa wana mwelekeo huo kwa Mungu, bado uongozi wa Mungu kwao hauachani na kanuni Zake; Anawaongoza kwa njia ya utaratibu kulingana na kanuni Zake na tabia Yake. Je, Mungu anauchukuliaje uhasama wao? Kama ujinga! Na kwa hiyo Amewasababisha hawa watu—wengi wa wasioamini—wakati mmoja kuwahi kupata mwili kama wanyama. Basi wasioamini ni nini machoni mwa Mungu? Wao ni mifugo. Mungu anaongoza mifugo na kwa watu kama hao Ana kanuni sawa. Hata kwa utawala wa Mungu kwa watu hawa, tabia Yake kwao, bado inaweza kuonekana, kama inavyowezekana sheria Zake kama chanzo cha utawala Wake juu ya vitu vyote. Hivyo basi, unaona mamlaka ya Mungu katika

kanuni ambazo kwazo Anawaongoza wasioamini ambao Nimezungumzia hivi punde? Je, mnaona tabia ya haki ya Mungu? (Tunaona.) Yaani, haijalishi Anashughulikia kitu gani kati ya vitu vyote Anavyoshughulikia, Mungu anatenda kulingana na kanuni na tabia Yake. Hiki ndicho kiini cha Mungu. Hangeweza kujitenga kiholela na amri au sheria za mbinguni Alizozipanga kwa sababu Anamwona mtu wa aina hii kama mfugo. Mungu anatenda kulingana na kanuni, bila kuzivuruga hata kidogo, matendo Yake hayaathiriwi na jambo lolote, na haijalishi Anafanya nini, yote ni kulingana na kanuni Zake mwenyewe. Hili ni kwa sababu Mungu ana kiini cha Mungu Mwenyewe, ambacho ni kipengele cha kiini Chake ambacho hakimo kwenye kiumbe yeyote. Mungu ni Mwangalifu na Anawajibika katika kushughulikia Kwake, njia Zake, usimamizi, uongozi, na utawala wa kila chombo, mtu, na kiumbe hai miongoni mwa vitu vyote Alivyoumba, na Hajawahi kuwa mzembe katika hili. Yeye ni mwenye neema na mkarimu kwa wale walio wazuri; Kwa wale waovu, Anawapa adhabu bila huruma; na kwa viumbe hai mbalimbali, Anafanya mipango ifaayo kwa wakati na kwa njia ya kawaida kulingana na mahitaji mbalimbali ya ulimwengu wa wanadamu katika nyakati mbalimbali, kiasi kwamba hawa viumbe hai mbalimbali wanapata miili kulingana na nafasi wanayochukua kwa njia ya utaratibu, na kuhama kati ya ulimwengu yakinifu na ulimwengu wa kiroho kwa njia ya utaratibu.

Kifo cha kiumbe hai—kuondokewa na uhai wa kimwili—kinaashiria kwamba kiumbe hai huyu ametoka katika ulimwengu yakinifu hadi ulimwengu wa kiroho, ilhali kuzaliwa kimwili kunaashiria kwamba kiumbe hai ametoka ulimwengu wa kiroho na kuja ulimwengu yakinifu kuanza kufanya kazi yake, kuchukua nafasi yake. Iwe ni kuondoka au kuwasili kwa kiumbe, vyote havitenganishwi na kazi ya ulimwengu wa kiroho. Mtu akija katika ulimwengu yakinifu, mipango kabambe na fafanuzi huwa tayari imetengenezwa na Mungu katika ulimwengu wa kiroho kuhusu atakwenda katika familia gani, atafikia enzi gani, atawasili saa ngapi, na nafasi yake. Hivyo basi, maisha yote ya mtu huyu—mambo afanyayo, na njia azichukuazo—yanasonga kulingana na mipango ya ulimwengu wa kiroho, bila hitilafu hata kidogo. Wakati ambapo maisha ya kiroho yanaisha, wakati huo, na namna na mahali ambapo yanaishia, ni wazi na yanaonekana katika ulimwengu wa kiroho. Mungu anatawala ulimwengu yakinifu, na Anatawala ulimwengu wa kiroho, na Hawezi kuchelewesha mzunguko wa kawaida wa uhai na mauti wa roho, wala Hawezi kufanya makosa katika mpangilio wa mzunguko wa uhai na mauti wa roho. Kila msimamizi katika nyadhifa rasmi katika ulimwengu wa kiroho anafanya majukumu yake na kufanya ambacho anapaswa kufanya, kulingana na maelezo na sheria za Mungu. Na kwa hiyo, katika ulimwengu wa wanadamu, kila tukio la kuonekana lishuhudiwalo na binadamu lina utaratibu, na halina vurugu yoyote. Haya yote ni kwa sababu ya utawala uliopangiliwa wa Mungu juu ya vitu vyote, hali kadhalika kwa sababu mamlaka ya Mungu yanatawala kila kitu, na kila kitu Anachokitawala kinajumuisha ulimwengu yakinifu ambamo mwanadamu anaishi,

aidha, ulimwengu wa kiroho usioonekana nyuma ya mwanadamu. Na kwa hiyo, ikiwa mwanadamu anataka kuwa na maisha mazuri, na anataka kuishi katika mazingira mazuri, hali kadhalika kupewa ulimwengu yakinifu mzima, mwanadamu sharti pia apatiwe ulimwengu wa kiroho, ambao hauwezi kuonekana kwa yeyote, ambao unaongoza kila kiumbe hai kwa niaba ya mwanadamu, na ambao una utaratibu. Basi, inaposemwa kwamba Mungu ndiye chanzo cha uhai kwa vitu vyote, je, hatujakuza ufahamu na uelewa wetu wa “vitu vyote”? (Ndiyo.)

2. Mzunguko wa Uhai na Mauti wa Watu Mbalimbali Wenye Imani

Tumemaliza kujadili mzunguko wa uhai na mauti wa kundi la kwanza, wasioamini. Hebu sasa tujadili ule wa kundi la pili, watu mbalimbali wenye imani. “Mzunguko wa uhai na mauti wa watu mbalimbali wenye imani” vilevile ni mada muhimu sana, na inafaa kwamba muwe na kiasi fulani cha uelewa wake. Kwanza, hebu tuseme ni imani gani “imani” kwa watu wa imani inaashiria: dini tano kuu za Uyahudi, Ukristo, Ukatoliki, Uisilamu, na Ubudha. Pamoja na wasioamini, watu ambao ni waumini katika hizi dini tano wanajumuisha idadi kubwa ya watu duniani. Miongoni mwa dini hizi tano, wale ambao wametengeneza ajira kutokana na imani yao ni wachache, lakini hizi dini zina waumini wengi. Waumini wake huenda sehemu tofauti wanapokufa. “Tofauti” na nani? Na wasioamini, watu wasiokuwa na imani, ambao tumemaliza kuzungumzia. Baada ya kufa, waumini wa hizi dini tano huenda mahali pengine, mahali tofauti na wasioamini. Lakini ni mchakato sawa. Ulimwengu wa kiroho pia utafanya uamuzi juu yao kutegemea yale yote waliyoyafanya kabla wafe, baadaye watatayarishwa ipasavyo. Lakini mbona hawa watu wanawekwa sehemu tofauti kutayarishwa? Kuna sababu muhimu ya hili. Na hii sababu ni gani? Nitawaambia kutumia mfano. Lakini kabla nifanye hivyo, mnaweza kuwa mkijiwazia: “Labda ni kwa sababu wana imani ndogo katika Mungu! Wao si wasioamini kabisa.” Hii ndiyo sababu mbona. Kuna sababu muhimu sana kwa wao kuwekwa mahali pengine.

Chukua Ubudha: Hebu Niwaambie ukweli. Mfuasi wa Budha, kwanza kabisa, ni mtu aliyebadili dini kwenda Ubudha, na ni mtu ajuaye imani yake ni nini. Mfuasi wa Budha akinyoa nywele zake na kuwa mtawa wa kiume au mtawa wa kike, hii inamaanisha kuwa amejitenga na mambo ya kidunia na kuacha nyuma ghasia ya dunia ya mwanadamu. Kila siku anakariri maandiko ya sutra na kuimba majina ya Budha, na kula chakula bila nyama, anaishi maisha ya kujinyima anasa za kimwili, na kupitisha siku zake ndani ya mwangaza baridi, na hafifu wa taa ya mafuta ya siagi. Anaishi maisha yake yote kwa njia hii. Maisha yake ya kimwili yaishapo, anatengeneza muhtasari wa maisha yake, ila mioyoni mwake hajui atakapoenda baada ya kufa, atakutana na nani, na atakuwa na hatima ya aina gani—mioyoni mwake hana uhakika na haya mambo. Hajafanya chochote zaidi ya kuishi bila mwelekeo maisha yake yote akiambatana na

imani, baadaye anaondoka duniani akiambatana na matamania na maadili asiyoyafahamu. Hiyo ndiyo tamati ya maisha yake ya kimwili anapoiaga dunia ya walio hai, na baada ya hapo, anarudi katika sehemu yake asilia katika ulimwengu wa kiroho. Kama mtu hutu atapata mwili na kurudi duniani kuendelea na kujikuza kwake kunategemea mienendo na kujikuza kwake kabla ya kifo chake. Ikiwa hakufanya kitu kibaya wakati wa uhai wake, atapata mwili haraka na kurudishwa duniani, ambapo atakuwa mtawa wa kiume au mtawa wa kike tena. Kulingana na utaratibu wa mara ya kwanza, mwili wake unajikuza wenyewe, baada ya hapo anakufa na kurudi katika ulimwengu wa kiroho, ambapo anatathminiwa, na baada ya hapo—ikiwa hakuna shida—anaweza kurudi tena katika ulimwengu wa wanadamu, na kuweza kubadili dini hadi Ubudha tena na kuendelea kujikuza. Baada ya kupata mwili mara tatu hadi mara saba, atarudi tena katika ulimwengu wa kiroho, ambapo anakwenda kila mara ambapo maisha yake ya kimwili yanamalizika. Ikiwa viwango na mienendo yake mbalimbali katika ulimwengu wa wanadamu inaambata na sheria za mbinguni za ulimwengu wa kiroho, basi atabaki huko kutoka wakati huu kuendelea; hatapata mwili tena kama mwanadamu; wala hakutakuwa na tishio la yeye kuadhibiwa kwa kutenda maovu duniani. Hatawahi kupitia tena mchakato huu. Badala yake, kulingana na hali zake, atachukua nyadhifa katika milki ya kiroho. Hili ndilo wafuasi wa Budha wanaliita “kufikia hali ya Ubudha.” Kufikia hali ya Ubudha hasa kunamaanisha kufanikiwa kama afisa wa ulimwengu wa kiroho, na baada ya hapo kutozaliwa tena katika mwili mpya ama kuwa katika hatari ya kuadhibiwa. Aidha, kunamaanisha kwamba hakuna kupata taabu tena ya kuwa mwanadamu baada ya kuzaliwa upya. Hivyo basi, bado kuna uwezekano wake kupata mwili tena kama mnyama? (La.) Hili linamaanisha kwamba anabaki kushika nafasi katika ulimwengu wa kiroho, na kamwe hatazaliwa upya. Huu ni mfano mmoja wa kufanikiwa kufikia hali ya Ubudha katika dini ya Ubudha. Na kuhusu wale ambao hawafanikiwi, baada ya wao kurudi katika ulimwengu wa kiroho, wanachunguzwa na kuthibitishwa na ofisa mhusika, ambaye anagundua kuwa ingawa wako hai, hawakujikuza kwa makini au kuwa makini katika kukariri maandiko ya sutra na kuimba majina ya Budha kama inavyotakiwa na dini ya Ubudha, na badala yake, walikuwa wametenda matendo mengi maovu na kujihusisha katika mienendo mingi mibaya. Basi katika ulimwengu wa kiroho hukumu inatolewa juu ya uovu wao, na baada ya hapo wana hakika ya kuadhibiwa. Hakuna vighairi katika hili. Basi, mtu kama huyu atafanikiwa lini? Katika maisha ambamo hakutenda maovu yoyote—wakati, baada ya kurudi katika ulimwengu wa kiroho, inaonekana hakufanya chochote kibaya kabla afariki. Basi anaendelea kuzaliwa upya, akiendelea kukariri maandiko ya sutra na kuimba majina ya Budha, akipitisha siku zake ndani ya mwangaza baridi na hafifu wa taa ya mafuta ya siagi, bila kuua chochote chenye uhai, bila kula nyama, na hafurahii ulimwengu wa mwanadamu, akiachana na vurugu zake kabisa, na kuepuka migogoro na wengine. Katika mchakato huu, hafanyi maovu, na kufuatia hayo anarudi katika ulimwengu wa kiroho, na baada ya matendo na mienendo yake yote

kutathminiwa, anatumwa tena katika ulimwengu wa wanadamu, kwa mzunguko unaojirudia mara tatu au saba. Ikiwa hakuna kikwazo wakati huu, basi kupata kwake Ubudhaa hakutaathiriwa, na hakutacheleweshwa. Hii ni sifa ya mzunguko wa uhai na mauti wa watu wote wenye imani: Wanaweza “kufanikiwa” na kushikilia wadhifa katika ulimwengu wa kiroho; hili ndilo linawafanya kuwa tofauti na wasioamini. Kwanza kabisa, wanapokuwa hai duniani, matendo ya wale wanaoweza kushika wadhifa katika ulimwengu wa kiroho ni yapi? Ni sharti wasifanye kabisa ovu lolote: ni lazima wasifanye mauaji, uchomaji, ubakaji, au wizi; wakifanya hila, udanganyifu, au ujambazi, basi hawawezi kufanikiwa. Yaani, wakiwa na uhusiano au ushirikishaji wowote na uovu, hawataweza kuepukana na adhabu ya ulimwengu wa kiroho. Ulimwengu wa kiroho unafanya mipango inayofaa kwa wafuasi wa Budha wanaofikia hali ya Ubudha: wanaweza kuteuliwa kusimamia wale ambao wanaonekana kuamini katika Ubudha, na yule Mzee aliye Angani, na wafuasi wa Budha watapewa mamlaka, wanaweza tu kuteuliwa kuwasimamia wasioamini, vinginevyo wanaweza kuwa wasimamizi wadogo sana. Ugavi huo unalingana na asili ya hizi roho. Huu ni mfano wa Ubudha.

Miongoni mwa dini tano tulizozungumzia, Ukristo ni maalum kiasi fulani. Ni nini maalum kuhusu Ukristo? Hawa ni watu wanaomwamini Mungu wa kweli. Je, inawezekanaje wale wanaomwamini Mungu wa kweli waorodheshwe hapa? Kwa sababu Ukristo ni aina ya imani, basi, bila shaka, unahusiana tu na imani—ni aina ya sherehe, aina ya dini, na kitu tofauti na imani ya wale wanaomfuata Mungu kweli. Kilichonifanya kuuorodhesha miongoni mwa hizi dini tano ni kwa sababu Ukristo umeshushwa hadi kiwango sawa na Uyahudi, Ubudha, Uislamu. Wakristo wengi hawaamini kuna Mungu, au kwamba Anatawala juu ya vitu vyote, seuze kuamini katika uwepo Wake. Badala yake, wanatumia tu Maandiko Matakatifu kuzungumza kuhusu elimu ya dini, wakitumia elimu ya dini kuwafundisha watu kuwa wema, kuvumilia mateso, na kufanya vitu vizuri. Ukristo ni wa aina hiyo ya dini: Unazingatia tu nadharia za mafundisho ya kidini, hauna kabisa uhusiano wowote na kazi ya Mungu ya kusimamia na kuokoa wanadamu, ni dini ya wale wanaomfuata Mungu ambayo haitambuliwi na Mungu. Lakini pia Mungu ana kanuni kuhusu mtazamo Wake kwao. Hawatendei na kuwashughulikia wapendavyo bila mpango, njia sawa na wasioamini. Mtazamo Wake kwao ni sawa na Alio nao kwa wafuasi wa Budha: Ikiwa, angali hai, Mkristo anajiheshimu, anaweza kuzifuata kabisa Amri Kumi za Mungu na kuzingatia sheria na amri katika mahitaji yao kwa tabia zao wenyewe—na ikiwa wanaweza kufanya hivi katika maisha yao yote—basi pia watalazimika kuchukua muda sawa kupitia mzunguko wa uhai na mauti kabla hawajaweza kweli kupata huko kuitwako kuchukuliwa kuenda mbinguni. Baada ya kupata huku kunyakuliwa wanabaki katika ulimwengu wa kiroho, ambapo wanashika wadhifa na kuwa miongoni mwa wasimamizi. Vivyo hivyo, wakifanya maovu duniani, ikiwa ni watenda dhambi na kufanya dhambi nyingi, basi haiepukiki

kwamba wataadhibiwa kwa ukali unaotofautiana. Katika Ubudha, kufanikiwa kunamaanisha kufika kwa Nchi Safi ya Furaha Kubwa Sana, lakini hii inaitwaje katika Ukristo? Inaitwa “kuingia mbinguni” na “kunyakuliwa.” Wale ambao kwa kweli “wananyakuliwa” pia wanapitia mzunguko wa uhai na mauti mara tatu hadi saba, halafu, wakiwa wamekufa, wanaingia katika ulimwengu wa kiroho, kana kwamba walikuwa usingizini. Ikiwa walikuwa wanafaa wanaweza kusalia kushika wadhifa, na tofauti na watu walio duniani, hawatapata mwili kwa njia rahisi, au kulingana na mazoea.

Miongoni mwa dini hizi zote, mwisho zinaozungumzia na ambao zinajitahidi kufikia ni sawa na kufanikiwa katika Ubudha; ni vile tu “kufanikiwa” huku kunatimizwa kwa njia tofauti. Wote ni wa aina moja. Kwa hili kundi la watu wa dini hizi ambao wanaweza kufuata kabisa maadili ya kidini katika tabia zao, Mungu huwapa hatima nzuri, sehemu nzuri ya kwenda, na kuwatendea inavyofaa. Haya yote ni sawa, ila si jinsi ambavyo watu wanadhani, sawa? Sasa, baada ya kusikia kuhusu yanayowatokea watu katika Ukristo, mnahisi vipi? Je, mnahisi kwamba shida zao si za haki? Mnawahurumia? (Kidogo.) Hakuna kitu kinachoweza kufanywa; watajilaumu wenyewe. Kwa nini Ninasema hivi? Kazi ya Mungu ni ya kweli; Yeye yu hai na kweli, na kazi Yake inawalenga wanadamu wote na kila mmoja. Kwa nini basi wasikubali hili? Ni kwa nini wanampinga kwa nguvu na kumtesa Mungu? Wana bahati hata kuwa na mwisho kama huu, basi mbona mnawaonea huruma? Kwa wao kutendewa namna hii kunaonyesha uvumilivu mkubwa. Kulingana na kiasi ambacho wanampinga Mungu, wanapaswa kuangamizwa—bali Mungu hafanyi hili, anaushughulikia Ukristo sawa tu na dini ya kawaida. Sasa kuna haja ya kutoa maelezo ya kina kuhusu dini nyinginezo? Maadili ya dini zote hizi ni kuwa watu wapitie shida zaidi, wasifanye maovu, watende mambo mema, wasiwaapize watu wengine, wasiwahukumu wengine, wajitenge na ugomvi, na wawe watu wazuri—mafundisho ya kidini mengi ni ya aina hii. Na kwa hiyo, kama hawa watu wa imani—hawa watu wa dini na madhehebu mbalimbali—wanaweza kufuata kabisa maadili ya kidini, basi hawatafanya makosa au dhambi nyingi wakati wangali duniani, na baada ya kupata mwili mara tatu hadi saba, basi kwa jumla watu hawa, watu ambao wanaweza kufuata kabisa maadili ya kidini, watabaki kushikilia wajibu katika ulimwengu wa kiroho. Na je, kuna watu wengi wa aina hii? (La, hakuna wengi.) Jibu lako linategemea nini? Si rahisi kutenda mazuri, au kufuata amri na sheria. Ubudha hauwaruhusu watu kula nyama—unaweza kufanya hilo? Ungepaswa kuvaa kanzu za kijivu na kukariri maandiko ya sutra na kuimba majina ya Budha katika hekalu la wafuasi wa Budha siku nzima, ungeweza kufanya hivyo? Haingekuwa rahisi. Ukristo una Amri Kumi za Mungu, amri na sheria, je, ni rahisi kufuata? Si rahisi! Chukua mfano wa kutowaapia wengine: Watu hawawezi kufuata hii amri. Kwa kushindwa kujizuia wenyewe, wanaapa—na baada ya kuapa hawawezi kurudisha kiapo, basi wanafanya nini? Usiku wanakiri dhambi zao. Wakati mwingine

baada ya kuwaapia wengine, bado kuna chuki mioyoni mwao, na hata wanazidi zaidi na kupanga ni lini watawadhuru. Kwa jumla, kwa wale wanaoishi katika hii imani iliyokufa, si rahisi kukosa kufanya dhambi au kutenda maovu. Na kwa hiyo, katika kila dini, ni watu wachache sana tu ndio wanaweza kufanikiwa kweli. Unadhani kwamba kwa sababu watu wengi sana wanafuata hizi dini, wengi wataweza kubaki kuchukua nafasi katika milki ya kiroho. Lakini si wengi hivyo, ni wachache tu ndio wanaweza kulifikia hili. Kwa jumla ni hayo tu kwa mzunguko wa uhai na mauti wa watu wenye imani. Kinachowatofautisha ni kwamba wanaweza kufanikiwa, na hiki ndicho kinawatofautisha na wasioamini.

3. Mzunguko wa Uhai na Mauti wa Wafuasi wa Mungu

Baada ya hayo, hebu tuzungumzie mzunguko wa uhai na mauti wa wale wanaomfuata Mungu. Hili linawahusu, hivyo kuweni makini. Kwanza, fikiria kuhusu ni makundi gani ambamo watu wanaomfuata Mungu wanaweza kugawika. (Wateule wa Mungu na watendaji huduma.) Kuna mawili: wateule wa Mungu na watendaji huduma. Kwanza tutazungumza kuhusu wateule wa Mungu, ambao ni wachache. “Wateule wa Mungu” inarejelea nini? Baada ya Mungu kuumba vitu vyote na baada ya kuwepo wanadamu, Mungu alichagua kundi la watu ambao walimfuata, na wanaitwa tu “wateule wa Mungu.” Kuna mipaka maalum na umuhimu katika uchaguzi wa Mungu wa watu hawa. Mipaka ni maalum kwa vile ilizuiliwa kwa wachache waliochaguliwa, ambao ni lazima waje Anapofanya kazi muhimu. Na umuhimu ni upi? Kwa kuwa wao ni kikundi kilichochaguliwa na Mungu, umuhimu ni mkubwa. Yaani, Mungu anataka kuwakamilisha watu hawa, na kuwafanya wawe wakamilifu, na baada ya kazi Yake ya usimamizi kuisha, Atawachukua watu hawa. Je, umuhimu huu si mkubwa? Kwa hiyo, hawa wateule ni wa umuhimu mkubwa kwa Mungu, kwa kuwa ni wale ambao Mungu anakusudia kuwapata. Lakini watendaji huduma—vyema, hebu tuachane na uamuzi uliokwisha kufanywa na Mungu, na kwanza tuzungumzie asili yao. Maana ya kawaida ya “mtendaji huduma” ni mtu anayehudumu. Wanaohudumu ni wa kupita; hawahudumu kwa muda mrefu, au milele, ila wanaajiriwa au kuandikwa kwa muda mfupi. Wengi wao wanachaguliwa kutoka miongoni mwa wasioamini. Wajapo duniani ndipo inapoamriwa kwamba watachukua nafasi ya watendaji huduma katika kazi ya Mungu. Wanaweza kuwa walikuwa mnyama katika maisha yao yaliyopita, lakini pia wanaweza kuwa walikuwa mmoja wa wasioamini. Hiyo ndiyo asili ya watendaji huduma.

Hebu turejee kwa wateule wa Mungu. Wanapokufa, wateule wa Mungu huenda sehemu fulani tofauti kabisa na wasioamini na watu mbalimbali wenye imani. Ni sehemu ambayo wanaambatana na malaika na wajumbe wa Mungu, na ambayo inaendeshwa na Mungu binafsi. Japo katika sehemu hii, wateule wa Mungu hawawezi kumwona Mungu kwa macho yao

wenyewe, si kama sehemu nyingine yoyote katika milki ya kiroho; ni sehemu ambayo hili kundi la watu huenda baada ya kufa. Wakifa, wao pia hupitia uchunguzi mkali kutoka kwa wajumbe wa Mungu. Na ni nini kinachochunguzwa? Wajumbe wa Mungu huchunguza njia zilizopitiwa na hawa watu katika maisha yao yote katika imani yao kwa Mungu, ikiwa waliwahi au hawakuwahi kumpinga Mungu wakati huo, au kumlaani, na ikiwa walitenda au hawakutenda dhambi mbaya au maovu. Uchunguzi huu unajibu swali la ikiwa mtu fulani ataondoka au atabaki. “Kuondoka” kunarejelea nini? Na “kubaki” kunarejelea nini? “Kuondoka” kunarejelea ikiwa, kulingana na mienendo yao, watabaki miongoni mwa madaraja ya wateule wa Mungu. “Kubaki” kunarejelea kuwa wanaweza kubaki miongoni mwa watu ambao wanafanywa na Mungu kuwa kamili katika siku za mwisho. Mungu ana mipango maalum kwa wale wanaobaki. Katika kila kipindi cha kazi Yake, Mungu atatuma watu kufanya kazi kama mitume au kufanya kazi ya kuyaamsha makanisa, au kuyahudumia. Lakini watu ambao wana uwezo wa kazi kama hizo hawapati miili mara kwa mara kama wasioamini, ambao wanazaliwa upya tena na tena; badala yake, wanarudishwa duniani kulingana na mahitaji na hatua ya kazi ya Mungu, na si wale wapatao mwili mara kwa mara. Je, kuna amri kuhusu ni lini wapate mwili? Je, wanakuja mara moja baada ya kila miaka michache? Je, wanakuja na hiyo haraka? Hawafanyi hivyo. Hii inategemea kazi ya Mungu, hatua ya kazi ya Mungu, na mahitaji Yake, na hakuna amri. Amri moja tu ni kwamba Mungu akifanya hatua ya mwisho ya kazi Yake katika siku za mwisho, wateule hawa wote watakuja. Wakija wote, hii itakuwa mara ya mwisho ambapo wanapata mwili. Na kwa nini hivyo? Hii inategemea matokeo yatakayopatikana katika hatua ya mwisho ya kazi ya Mungu—kwani katika hatua hii ya mwisho ya kazi, Mungu atawafanya wateule hawa kuwa kamili kabisa. Hili linamaanisha nini? Ikiwa, katika hii awamu ya mwisho, watu hawa watafanywa kuwa kamili, na kufanywa wakamilifu, basi hawatapata mwili kama awali; mchakato wa kuwa wanadamu utakamilika kabisa, sawa na mchakato wa kuzaliwa katika mwili mpya. Hili linawahusu wale watakaobaki. Je, wale ambao hawawezi kubaki huenda wapi? Wasioweza kubaki wanakuwa na sehemu mwafaka ya kwenda. Kwanza kabisa kwa sababu ya maovu yao, makosa waliyofanya, na dhambi walizofanya, wao pia wanaadhibiwa. Baada ya kuadhibiwa, Mungu atafanya mpango wawe miongoni mwa wasioamini, vinginevyo miongoni mwa watu mbalimbali wenye imani, kulingana na hali. Yaani, kuna hali mbili kwao: Moja ni, baada ya kuadhibiwa, labda kuishi miongoni mwa watu wa dini fulani wanapopata mwili tena, na nyingine ni kuwa wasioamini. Kama watakuwa wasioamini, basi watapoteza kila fursa. Lakini wakiwa watu wa imani—kwa mfano, wakiwa Wakristo—bado wangali na nafasi ya kurudi miongoni mwa madaraja ya wateule wa Mungu; kwa hili kuna uhusiano changamano sana. Kwa ufupi, ikiwa mmoja wa wateule wa Mungu atafanya kitu kitakachomkosea Mungu, wataadhibiwa sawa tu na watu wengine. Chukulia Paulo, kwa mfano, ambaye tulizungumzia awali. Paulo ni mfano wa wale wanaoadhibiwa. Je, mnapata picha ya yale ninayozungumzia? Je,

mipaka ya wateule wa Mungu ni ya kudumu? (Kwa kiasi kikubwa ni ya kudumu.) Kiasi kikubwa chake ni cha kudumu, lakini sehemu ndogo si ya kudumu. Kwa nini hivyo? Nimerejelea hapa sababu moja dhahiri: kutenda maovu. Wanapotenda maovu, Mungu hawataki, na wakati Mungu hawataki, anawatupa miongoni mwa makabila na aina mbalimbali za watu, kitu ambacho kinawaacha bila tegemeo na kufanya kurudi kwao kuwe kugumu. Haya yote yanahusu mzunguko wa uhai na mauti wa wateule wa Mungu.

Kinachofuata ni mzunguko wa uhai na mauti wa watendaji huduma. Tulizungumzia tu asili za watendaji huduma, yaani, walipata mwili kutoka kwa wasioamini na wanyama katika maisha yao ya awali. Na ujio wa hatua ya mwisho ya kazi, Mungu amechagua kundi la watu hawa kutoka kwa wasioamini, na ni kundi ambalo ni maalum. Nia ya Mungu ya kuchagua watu hawa ni kuhudumia kazi Yake. “Huduma” si neno la jamala kutamka, wala si kitu ambacho mtu yeyote angependa, lakini tunapaswa kuona ambao linawalenga. Kuna umuhimu maalum katika uwepo wa watendaji huduma wa Mungu. Hamna mwingine awezaye kuchukua nafasi yao, kwa kuwa walichaguliwa na Mungu. Na ni ipi nafasi ya watendaji huduma? Kuwahudumia wateule wa Mungu. Kwa ujumla, kazi yao ni kuhudumia kazi ya Mungu, kushirikiana na kazi ya Mungu, na kushirikiana na ukamilisho wa Mungu wa wateule Wake. Haijalishi kama wanafanya kazi ngumu, wanafanya kazi fulani, au wanajiandaa kufanya kazi fulani, ni yapi mahitaji ya Mungu kwa hawa watu? Je, anawadai sana kwa masharti Yake kwao? (La, Mungu anawataka wawe waaminifu.) Watendaji huduma pia wanapaswa kuwa waaminifu. Haijalishi asili zako, au kwa nini Mungu alikuchagua, ni lazima uwe mwaminifu kwa Mungu, kwa kile anachokuagiza, na vilevile kazi unayoiwajibikia na jukumu unalolifanya. Ikiwa watendaji huduma wanaweza kuwa waaminifu, na kumridhisha Mungu, basi hatima yao itakuwaje? Wataweza kubaki. Je, ni baraka kuwa mtendaji huduma anayebaki? Kubaki kunamaanisha nini? Hii baraka inamaanisha nini? Kihadhi, hawafanani na wateule wa Mungu, wanaonekana tofauti. Kwa hakika, hata hivyo, wakipatacho katika maisha haya siyo sawa na wakipatacho wateule wa Mungu? Angalau, katika haya maisha ni sawa. Hamlipingi hili, naam? Matamko ya Mungu, neema ya Mungu, riziki ya Mungu, baraka za Mungu—ni nani hafurahii vitu hivi? Kila mtu anafurahia wingi wa haya. Kitambulisho cha mtendaji huduma ni mtendaji huduma, lakini kwa Mungu, ni miongoni mwa vitu vyote Alivyoumba—tofauti ni kwamba tu nafasi yao ni ile ya watendaji huduma. Kama mmoja wa viumbe wa Mungu, kuna tofauti kati ya watendaji huduma na wateule wa Mungu? Kwa hakika, hakuna. Kwa mazungumzo ya kawaida, kuna tofauti, katika kiini kuna tofauti, kwa kurejelea nafasi wanazoshika kuna tofauti, ila Mungu hawabagui hawa watu. Hivyo ni kwa nini hawa watu wanatambuliwa kama watendaji huduma? Unapaswa kuelewa hili. Watendaji huduma wanatokana na wasioamini. Kutaja wasioamini kunatuambia kuwa maisha yao ya awali ni mabaya: Wote ni wakana Mungu, katika maisha yao ya nyuma walikuwa wakana Mungu,

hawakumwamini Mungu, na walikuwa mahasimu wa Mungu, wa ukweli, na vitu vizuri. Hawakumwamini Mungu, hawakuamini kuwa kuna Mungu, hivi wana uwezo wa kuelewa maneno ya Mungu? Ni haki kusema kwamba, kwa kiwango kikubwa, hawana. Sawa tu na wanyama wasivyo na uwezo wa kuelewa maneno ya mwanadamu, watendaji huduma hawaelewi Mungu anasema nini, Anahitaji nini, kwa nini Ana mahitaji kama hayo—hawaelewi, hivi vitu havieleweki kwao, wanabaki bila nuru. Na kwa sababu hii, watu hawa hawana uhai tuliozungumzia. Je, bila uhai, watu wanaweza kuelewa ukweli? Je, wana ukweli? Je, wana uzoefu na ufahamu wa maneno ya Mungu? (La.) Hizo ndizo asili za watendaji huduma. Lakini kwa kuwa Mungu anawafanya hawa watu watendaji huduma, bado kuna viwango Anavyohitaji wawe navyo; Hawadharau, na Hawachukulii kwa uzembe. Japo hawaelewi maneno yake, na hawana uhai, bado Mungu ni mwema kwao, na bado kuna viwango Anavyohitaji wawe navyo. Mmemezungumzia hivi viwango hivi karibuni: Kuwa mwaminifu kwa Mungu, na kufanya Asemacho. Katika huduma yako ni lazima uhudumu unapohitajika, na ni lazima uhudumu hadi mwisho. Ikiwa unaweza kuwa mtendaji huduma mwaminifu, unaweza kuhudumu hadi mwisho, na unaweza kutimiza agizo uliloaminiwa na Mungu kikamilifu, basi utaishi maisha ya thamani, na utaweza kubaki. Ukitia bidii kidogo, ukijaribu kwa nguvu, ukiongeza maradufu jitihada zako za kumjua Mungu, ukiweza kuongea kidogo kuhusu ufahamu wa Mungu, ukiweza kumshuhudia Mungu, na zaidi, ukielewa kitu kuhusu mapenzi ya Mungu, ukiweza kushirikiana katika kazi ya Mungu, na ukiyazingatia kidogo mapenzi ya Mungu, basi wewe, mtendaji huduma, utapata bahati. Na hili litakuwa badiliko gani katika bahati? Hutaweza kubaki tu. Kutegemea tabia yako na malengo na juhudi zako binafsi, Mungu atakufanya mmoja wa wateule. Hii itakuwa bahati yako. Kwa watendaji huduma, ni nini kizuri kuhusu hili? Ni kwamba unaweza kuwa mmoja wa wateule wa Mungu. Wakiwa mmoja wa wateule wa Mungu, inamaanisha kuwa hawatapata tena mwili kama wanyama au wasioamini. Je, hiyo ni habari njema? Ndiyo, na ni habari njema. Inamaanisha, watendaji huduma wanaweza kufinyangwa. Si kwamba kwa mtendaji huduma, Mungu akimpangia awali kuhudumu, daima atahudumu; si lazima iwe hivyo. Kutegemea tabia yake binafsi, Mungu atamtendea tofauti, na kumjibu tofauti.

Lakini kuna watendaji huduma ambao hawana uwezo wa kumtumikia Mungu hadi mwisho; wakati wa huduma yao, kuna wale ambao wanajitoa nusu na kutelekeza Mungu, kuna wale ambao hufanya mambo mengi mabaya, na hata wale ambao wanasababisha madhara makubwa na kufanya uharibifu mkubwa kwa Kazi ya Mungu, kuna hata watendaji huduma ambao humlaani Mungu, na kadhalika—na ni nini maana ya matokeo haya yasiyorekebishika? Matendo maovu yoyote kama hayo humaanisha kufikia mwisho kwa huduma yao. Kwa sababu matendo yako wakati wa huduma yamekuwa maovu sana, kwa sababu umevuka mipaka yako, wakati Mungu anaona huduma yako haijafikia kiwango Atakutoa ustahiki wa kutoa huduma, Hatakubali

ufanye huduma, Atakutoa mbele ya macho Yake, na kutoka katika nyumba ya Mungu. Au ni kwamba hutaki kufanya huduma? Je, siku zote hutamani kufanya maovu? Je, siku zote wewe si mwaminifu? Sawa basi, kuna suluhisho rahisi: Utanyang'anywa ustahiki wako wa kuhudumu. Kwa Mungu, kunyang'anya mtendaji huduma ustahiki wa kufanya huduma kuna maana kuwa mwisho wa mtendaji huduma huyu umetangazwa, na hatakuwa anastahili kufanya huduma kwa Mungu tena, Mungu hahitaji huduma zake tena, na haijalishi ni vitu vipi vizuri atasema, maneno haya yatabaki ya bure. Mambo yanapofikia kiwango hiki, hii hali itakuwa isiyorekebisha; watendaji huduma kama hawa hawana njia ya kurudi nyuma. Na Mungu huwafanyia nini watendaji huduma kama hawa? Anawaachisha tu kutoa huduma? La! Je, Anawazuia tu wasibaki? Au anawaweka katika upande mmoja. Na kuwangoja wabadilike? Hafanyi hivyo. Kwa kweli Mungu hana upendo sana kwa watendaji huduma. Iwapo mtu ana aina hii ya mwelekeo katika huduma yake kwa Mungu, Mungu, kutokana na matokeo ya mwelekeo huu, Atamnyang'anya ustahiki wake wa kutoa huduma, na kwa mara nyingine tena kumtupa miongoni mwa wasioamini. Na ni ipi hatima ya watendaji huduma waliorudishwa tena kati ya wasioamini? Ni sawa na ile ya wasioamini; kupata mwili kama wanyama na kupokea adhabu ya wasioamini katika ulimwengu wa kiroho. Na Mungu hatakuwa na maslahi ya kibinafsi katika adhabu yao, kwa kuwa hawana umuhimu wowote tena katika kazi ya Mungu. Huu si mwisho tu wa maisha yao ya imani kwa Mungu, ila mwisho wa hatima yao pia, kutangazwa kwa hatima yao. Kwa hiyo watendaji huduma wakihudumu vibaya, watapata matokeo wao wenyewe. Kama mtendaji huduma hana uwezo wa kufanya huduma hadi mwisho kabisa, au amenyang'anywa ustahiki wake wa kutoa huduma katikati ya njia, basi watatupwa miongoni mwa wasioamini—na kama watatupwa miongoni mwa wasioamini watashughulikiwa sawa na jinsi mifugo wanavyoshughulikiwa, sawa na watu wasio na akili au urazini. Ninapoelezea namna hiyo, unaelewa, naam?

Ilivyo hapo juu ndivyo Mungu anavyoshughulikia mzunguko wa uhai na mauti wa wateule wake na watendaji huduma. Mnajihisi vipi baada ya kusikia haya? Nimewahi kuzungumza kuhusu mada ambayo Nimeitaja sasa hivi, mada ya wateule wa Mungu na watendaji huduma? Kwa kweli Nimewahi, lakini hamkumbuki. Mungu ni mwenye haki kwa wateule wake na watendaji huduma. Kwa vyovyote vile Yeye ni mwenye haki, siyo? Kuna mahali popote unaweza kupata makosa? Wapo watu ambao watasema: “Kwa nini Mungu ni mvumilivu sana kwa wateule? Na kwa nini anawavumilia kidogo sana watendaji huduma?” Kuna yeyote angependa kuwatetea watendaji huduma? “Je, Mungu anaweza kuwapa watendaji huduma muda zaidi, na kuwa mstahimilivu na mvumilivu zaidi kwao?” Haya maneno yako sahihi? (Hapana, hayapo sahihi.) Na ni kwa nini hayapo sahihi? (Kwa kuwa tumeonyeshwa neema kweli kwa kufanywa kuwa watendaji huduma.) Watendaji huduma wameonyeshwa neema kwa kuruhusiwa

kufanya huduma! Bila ya dhana “watendaji huduma,” na bila Kazi ya watendaji huduma, hawa watendaji huduma wangukuwa wapi? Miongoni mwa wasioamini, wakiishi na kufa pamoja na mifugo. Ni neema kubwa wanayoifurahia leo, kuruhusiwa kuja mbele za Mungu, na kuja katika nyumba ya Mungu! Hii ni neema kubwa! Kama Mungu hakukupa nafasi ya kutoa huduma, usingekuwa na nafasi ya kuja mbele za Mungu. Kwa kusema machache, hata kama wewe ni Mbudha na umefanikiwa, sanasana wewe ni mtumwa katika ulimwengu wa kiroho; hutaweza kamwe kumwona Mungu, au kusikia sauti Yake, au kusikia maneno Yake, au kuhisi upendo Wake na baraka Zake kwako, na hata isingewezekana kamwe kuonana na Yeye uso kwa uso. Kilicho tu mbele ya wafuasi wa Budha ni kazi rahisi. Hawawezi kamwe kumjua Mungu, na wanaitikia na kutii kiupofu tu, wakati ambapo watendaji huduma wanafaidi mengi sana katika hatua hii ya kazi. Kwanza, wanaweza kuonana na Mungu uso kwa uso, kusikia sauti Yake, kuyasikia maneno Yake, na kupitia neema na baraka Anazowapa watu. Aidha, wanaweza kufurahia maneno na ukweli unaopewa na Mungu. Watendaji huduma kwa kweli hupata mengi zaidi! Basi, kama mtendaji huduma, huwezi hata kutia juhudi inayofaa, je, Mungu bado atakuweka? Hawezi kukuweka. Hataki mengi kutoka kwako lakini hufanyi chochote Anachotaka vizuri, hujawajibika ipasavyo—na kwa hivyo, bila shaka, Mungu hawezi kukuweka. Hiyo ndiyo tabia ya haki ya Mungu. Mungu hakudekezi, lakini wala Hakubagui. Mungu anafanya kazi na kanuni hizo. Mungu hutekeleza mambo jinsi hii kwa watu na viumbe wote.

Inapokuja katika ulimwengu wa kiroho, kama viumbe mbalimbali waliomo watafanya kitu kibaya, kama hawafanyi kazi yao inavyostahili, Mungu pia ana sheria za peponi na amri zifaazo kuwashughulikia—hili halipingwi. Basi, katika maelfu kadhaa ya miaka ya kazi ya usimamizi ya Mungu, wasimamizi wengine ambao walifanya maovu wameangamizwa, wengine, leo, wangali wanazuiliwa na kuadhibiwa. Hili ndilo linafaa kukabiliwa na kila kiumbe aliye katika ulimwengu wa kiroho. Akifanya kitu kibaya au kutenda maovu, anaadhibiwa—ambayo ni sawa na jinsi Mungu anavyotenda kwa wateule Wake na watendaji huduma. Na kwa hivyo, iwe ni katika ulimwengu wa kiroho au ulimwengu yakinifu, kanuni ambazo Mungu hutekeleza matendo hazibadiliki. Bila kujali kama unaweza kuona matendo ya Mungu au la, kanuni zao hazibadiliki. Daima, Mungu amekuwa na kanuni sawa kwa jinsi Anavyotekeleza matendo kwa vitu vyote na kuvishughulikia vitu vyote. Hili halibadiliki. Mungu atakuwa mkarimu kwa wale walio miongoni mwa wasioamini ambao angalau wanaishi ipasavyo, na kuwapa nafasi wale walio katika kila dini ambao wana tabia nzuri na hawatendi maovu, kwa kuwaruhusu kutekeleza wajibu wao katika vitu vyote vinavyosimamiwa na Mungu, na kufanya kile ambacho wanafaa kufanya. Vivyo hivyo, kati ya wale wanaomfuata Mungu, kati ya wateule Wake, Mungu habagui mtu yeyote kulingana na kanuni Zake hizi. Ni mwema kwa kila mtu anayeweza kumfuata kwa dhati, na kupenda kila mtu anayemfuata kwa dhati. Ni kwamba tu kwa aina hizi mbalimbali za

watu—wasioamini, aina tofauti za watu wenye imani, na wateule wa Mungu—anachowazawadia wao ni tofauti. Chukulia wasioamini: hata kama hawamwamini Mungu, na Mungu huwaona kama mifugo, miongoni mwa kila kitu kila mmoja wao ana chakula, mahali pao wenyewe, na mzunguko wa kawaida wa uhai na mauti. Wanaotenda maovu wanaadhibiwa, na wanaofanya mazuri wanabarikiwa na hupokea wema wa Mungu. Hivyo ndivyo ilivyo? Kwa watu wenye imani, kama wanaweza kutii hasa maadili ya kidini, kizazi baada ya kizazi, basi baada ya hivi vizazi vyote Mungu hatimaye atatoa uamuzi Wake kwao. Vivyohivyo, kwa wewe leo, awe mmoja wa wateule wa Mungu au mtendaji huduma, Mungu vilevile atakuwazisha na kuamua mwisho wako kulingana na kanuni na amri za utawala ambazo Ameziweka. Miongoni mwa aina hizi kadhaa za watu—aina tofauti za watu wa imani, walio katika dini tofauti—je, Mungu amewapa nafasi ya kuishi? Uko wapi Uyahudi? Mungu ameingilia katika imani yao? Hajaingilia, siyo? Na vipi kuhusu Ukristo? Hajaingilia pia? Anawaruhusu kufuata mipangilio yao wenyewe, na Hasemi nao, au kuwapa nuru yoyote, na, zaidi ya hayo, Hawafichulii kitu chochote: “Kama unafikiria ni sahihi, basi amini hivyo.” Wakatoliki wanamwamini Maria, na kwamba ni kupitia kwa Maria ambapo habari zilimfikia Yesu; hiyo ndiyo aina yao ya imani. Na Mungu amewahi kurekebisha imani yao? Mungu huwapa uhuru, Mungu hawasikizi, na huwapa sehemu fulani ambapo wataishi. Na kwa Waisilamu na wafuasi wa Budha, je, Yuko hivyo pia? Ameweka mipaka kwa ajili yao, pia, na kuwaruhusu kuwa na mahali pao wenyewe pa kuishi, bila ya kuingilia imani zao. Yote yamepangwa vizuri. Na unaona nini katika haya yote? Kwamba Mungu ana mamlaka, lakini hatumii vibaya mamlaka Yake. Mungu hupanga vitu vyote katika mpangilio taratibu, na ni mwenye utaratibu, na katika hili busara na kudura Zake vinadhihirika.

Leo tumezungumzia mada mpya na maalum, ambayo inahusu masuala ya ulimwengu wa kiroho, ambayo ni sehemu mojawapo ya uendeshaji na utawala wa Mungu juu ya ulimwengu wa kiroho. Mlipokuwa hamyaelewi mambo haya, huenda mlisema; “Chochote kinachohusiana na haya ni mafumbo, na hayahusiani na kuingia kwetu katika uhai; mambo haya yametenganishwa na jinsi watu wanaishi hasa, na hatutaki kuyaelewa, wala hatutamani kuyasikia. Hayana uhusiano wowote na kumfahamu Mungu.” Sasa, mnafikiria kuna shida na aina hiyo ya mawazo? Ni sahihi? (La.) Mawazo kama hayo sio sahihi, na yana matatizo makubwa. Hii ni kwa sababu, kama unatamani kujua jinsi Mungu anatawala juu ya vitu vyote, huwezi tu kuelewa kile ambacho unaweza kuona na kile unachokipata kutoka kwa mawazo yako. Ni lazima pia ufahamu ya ulimwengu ule mwingine ambao hauonekani kwako, ambao umeunganishwa kwa njia isiyochanganulika na huu ulimwengu ambao unaweza kuuona. Haya yanahusu ukuu wa Mungu, yanahusu mada ya “Mungu ndiye chanzo cha uhai kwa vitu vyote”; ni taarifa kuhusu hayo. Bila ya hii taarifa, kungekuwepo na dosari na upungufu katika ufahamu kuhusu jinsi Mungu alivyo chanzo cha uhai kwa vitu vyote. Hivyo, kile ambacho tumeongea leo kinaweza kusemwa kuwa

kimetamatisha yale tuliyoyaongelea kabla, pamoja na maudhui ya “Mungu ndiye chanzo cha uhai kwa vitu vyote.” Baada ya kuelewa haya, mna uwezo wa kumjua Mungu kupitia maudhui haya? Na kilicho muhimu zaidi ni kwamba leo, Nimewapitisha ujumbe muhimu sana: kuhusu watendaji huduma. Ninajua mnapenda sana kusikia mada kama hizi, kwamba mnayatilia maanani sana mambo haya, basi mnahisi mmeridhika na yale Nimezungumzia leo? (Ndiyo, tumeridhika.) Mwaweza kuwa hamvutiwi sana na vitu vingine, lakini haswa mnavutiwa na mazungumzo kuhusu watendaji huduma, kwa kuwa hii mada inagusia kila moyo wa mmoja wenu.

Mahitaji ya Mungu kwa Wanadamu

1. Utambulisho na Hadhi ya Mungu Mwenyewe

Tumefikia mwisho wa mada ya “Mungu ni chanzo cha uhai kwa vitu vyote,” vilevile na ile ya “Mungu ni wa kipekee Mungu Mwenyewe.” Baada ya kufanya hivyo, tunahitaji kufanya muhtasari. Muhtasari wa aina gani? Unaomhusu Mungu Mwenyewe. Kwa kuwa ni kumhusu Mungu Mwenyewe, basi lazima ugusie kila kipengele cha Mungu, vilevile aina ya imani ya watu kwa Mungu. Na kwa hiyo, kwanza lazima Niwaulize: Baada ya kusikia mahubiri, Mungu ni nani katika jicho la mawazo yako? (Muumbaji.) Mungu katika jicho la mawazo yako ndiye Muumbaji. Kuna kitu kingine chochote? Mungu ni Bwana wa vitu vyote. Maneno haya yanafaa? (Yanafaa.) Mungu ndiye mtawala wa vitu vyote, na anayeendesha vitu vyote. Aliumba vitu vyote, Anaendesha vitu vyote, na pia Anatawala vitu vyote na kukimu vitu vyote. Hii ndiyo hadhi ya Mungu, na utambulisho wa Mungu. Kwa vitu vyote na vyote vilivyopo, utambulisho wa kweli wa Mungu ni Muumbaji, na Mtawala wa vitu vyote. Huo ni utambulisho unaomilikiwa na Mungu, na ni wa kipekee miongoni mwa vitu vyote. Hakuna Kati ya viumbe wa Mungu—wawe miongoni mwa wanadamu, au katika ulimwengu wa kiroho—ambao wanaweza kutumia namna yoyote au kisingizio kuiga au kuchukua nafasi ya utambulisho wa Mungu na hadhi Yake, kwa kuwa kuna mmoja tu kati ya vitu vyote anayemiliki huu utambulisho, nguvu, mamlaka, na uwezo wa kutawala vitu vyote: Mungu wetu wa kipekee Mwenyewe. Anaishi na kutembea miongoni mwa vitu vyote; Anaweza kufikia palipo mbali zaidi, juu ya vitu vyote; Anaweza kunyenyekea kwa kuwa mwanadamu, kuwa mmoja wa wenye mwili na damu, kuonana ana kwa ana na watu na kushiriki na wao dhiki na faraja; wakati huo huo, Anaamuru vitu vyote, na Huamua hatima ya vitu vyote, na njia itakayofuata, zaidi na hayo, Anaongoza hatima za wanadamu wote, na njia za wanadamu. Mungu kama huyu anastahili kuabudiwa, kuheshimiwa, na kujulikana na viumbe wote. Na hivyo, pasipo kujali uko katika kundi na aina gani ya wanadamu, kumwamini Mungu, kumfuata Mungu, kumheshimu Mungu sana, kukubali utawala wa Mungu, na kukubali mipango ya Mungu katika hatima yako ndio uamuzi wa pekee, na

uamuzi unaofaa, kwa mtu yeyote, kwa kiumbe chochote kinachoishi. Katika upekee wa Mungu, watu huona kwamba mamlaka Yake, tabia Yake ya haki, kiini Chake, na namna ambazo Anakirimia vitu vyote ni za kipekee; upekee Wake unabainisha utambulisho wa kweli wa Mungu Mwenyewe, na unabaini hadhi Yake. Na kwa hivyo, miongoni mwa viumbe vyote, kama kuna kiumbe anayeishi katika ulimwengu wa kiroho au miongoni mwa wanadamu angetamani kusimama badala ya Mungu, haingewezekana, sawa na kujaribu kumuiga Mungu. Huu ni ukweli. Ni mahitaji yapi kwa mwanadamu aliyonayo Muumbaji na Mtawala kama huyu, ambaye Aliye na utambulisho, nguvu, na hadhi ya Mungu Mwenyewe? Hili linapaswa kuwa wazi kwa kila mtu, na linapaswa kukumbukwa nanyi, na ni muhimu sana kwa Mungu na mwanadamu!

2. Mielekeo Mbalimbali ya Wanadamu kwa Mungu

Jinsi watu wamtendeavyo Mungu huamua hatima yao, na huamua jinsi Mungu anavyowatendea na kuwashughulikia. Kufikia sasa nitawapa mifano kadhaa ya jinsi watu wanavyotenda mbele za Mungu. Hebu tusikie kitu kuhusu ama mienendo na tabia ambazo kwazo wanamtendea Mungu ni sahihi au la. Hebu tuangalie mwenendo wa aina saba za watu wafuatao:

1) Kuna aina moja ya watu ambao mwelekeo wao kwa Mungu haswa ni wa kipuuzi. Wanafikiria kuwa Mungu ni kama Bodhisattva au kiumbe takatifu wa masimulizi ya kibinadamu, na kuwataka watu kusujudu mara tatu wanapokutana na kuchoma ubani baada ya kula. Kwa hivyo, katika mioyo yao, wanapomshukuru Mungu kwa neema Yake, na kuwa wenye shukrani kwa Mungu, mara nyingi wana msukumo kama huo. Hivyo wanatamani Mungu wanaomwamini leo, kama kiumbe takatifu wanayemtamania ndani ya mioyo yao, anaweza kukubali mienendo yao Kwake ambapo wanasujudu mara tatu wanapokutana, na kuchoma ubani baada ya kula.

2) Watu wengine wanamwona Mungu kama Budha anayeishi, mwenye uwezo wa kutoa wanaoishi wote kutoka kwenye mateso, na kuwaokoa; wanaona Mungu kama Budha anayeishi mwenye uwezo wa kuwatoa kwenye mateso mengi. Imani ya watu hawa kwa Mungu ni kumwabudu Mungu kama Buddha. Ijapokuwa hawachomi ubani, kusujudu, au kutoa sadaka, katika nyoyo zao Mungu ni kama tu Buddha, na huwataka tu wawe wema na wenye huruma, kuwa wasiue chochote kilicho hai, wasiwaapie wengine, waishi maisha yanayoonekana kuwa manyoofu, na wasifanye chochote kibaya—vitu hivi tu. Huyu ndiye Mungu mioyoni mwao.

3) Watu wengine humwabudu Mungu kama mtu mkubwa au maarufu. Kwa mfano, kwa namna yoyote mtu huyu mkubwa hupenda kuongea, kwa kiimbo chochote huongea, maneno na msamiati anaotumia, kiimbo chake, ishara zake za mikono, maoni na matendo yake, ukali wake—wanaiga yote, na hivi ndivyo vitu ambavyo ni lazima watavisababisha katika mwendo wa

imani yao kwa Mungu.

4) Watu wengine wanamwona Mungu kama mfalme, wanahisi kuwa Yuko juu ya vitu vyote vingine, na hakuna anayejaribu kumkosea—na wakifanya hivyo, wataadhibiwa. Wanaabudu mfalme kama huyo kwa sababu wafalme huwa wanashikilia sehemu fulani kwenye mioyo yao. Mawazo, tabia, mamlaka, na asili ya wafalme—hata na maslahi na maisha yao ya kibinafsi—yote huwa kitu ambacho watu hawa lazima waelewe, masuala na mambo ambayo wanashughulika nayo, na hivyo wanamwabudu Mungu kama mfalme. Imani ya namna hiyo inachekesha.

5) Watu wengine wana imani fulani katika uwepo wa Mungu, ambayo ni kubwa na isiyotingishika. Kwa sababu ufahamu wa Mungu kwao ni wa juujuu mno na hawana mazoea ya maneno ya Mungu, wanamwabudu kama sanamu. Sanamu hii ni Mungu aliye ndani ya mioyo yao, ni kitu ambacho wanafaa kuogopa na kusujudia, na ambayo wanalazimika kufuata na kuiga. Wanamwona Mungu kama sanamu, ambayo wanafaa kufuata maisha yao yote. Wanaiga sauti ambayo kwayo Mungu huzungumza, na kwa nje wanaiga wale ambao Mungu anapenda. Aghalabu wanafanya mambo ambayo yanaonekana kuwa manyoofu, safi, na ya kweli, na wanafuata hii sanamu kama mwenzao au mwandani wao ambaye wanaweza kushirikiana. Hiyo ndiyo aina ya imani yao.

6) Kuna watu ambao, kando na kusoma maneno mengi ya Mungu na kuwa wameyasikia mahubiri mengi, wanahisi ndani ya nyoyo zao kuwa msimamo tu wa mienendo yao kwa Mungu ni kuwa kila wakati wanafaa wawe watiifu na kujipendekeza, la sivyo wanafaa kumsifu Mungu na kumwabudu kwa njia isiyo halisi. Wanaamini kuwa Mungu ni Mungu anayewahitaji kutenda hivyo, na wanaamini kuwa wasipofanya hivyo, basi wakati wowote wanaweza kuchochea hasira Yake au kumtenda dhambi, na kwamba kwa sababu ya kutenda dhambi Mungu atawaadhibu. Huyu ndiye Mungu mioyoni mwao.

7) Kisha kuna watu wengi, wanaotafuta riziki ya kiroho katika Mungu. Kwa sababu wanaishi katika ulimwengu huu, hawana amani au furaha, na hakuna wanapopata faraja. Baada ya kumpata Mungu, wanapokuwa wameona na kusikia maneno Yake, ndani ya mioyo yao wanafurahi na kuisimka kisiri. Hii ni kwa sababu wanaamini kuwa tayari wamepata mahali ambapo patawapa furaha, kwamba hatimaye wamepata Mungu ambaye atawapa riziki ya kiroho. Baada ya kukubali Mungu na kuanza kumfuata, wanakuwa wenye furaha, maisha yao yanakamilishwa, hawako kama wengine wasioamini tena, wanaotembea usingizini maishani mwao kama wanyama, na wanahisi kuwa kuna kitu cha kutamania katika maisha. Kwa hivyo, wanafikiri kuwa huyu Mungu anaweza kuwatimizia mahitaji yao ya kiroho na kuleta furaha kubwa katika mawazo na Roho. Bila ya kujua, wanakuwa hawawezi kumwacha huyu Mungu

anayewapa riziki ya kiroho, Anayeleta furaha katika Roho na familia zao. Wanaamini kuwa imani katika Mungu haihitaji zaidi ya kuwapa riziki ya kiroho.

Je, mielekeo kumwelekea Mungu ya watu hawa wa aina mbalimbali waliotajwa hapo juu ipo miongoni mwenu? (Ipo.) Kama, katika imani yao katika Mungu, moyo wa mtu una mwelekeo wowote kati ya hii, je, kweli wanaweza kuja mbele za Mungu? Kama watu wana mwelekeo wowote kati ya hii katika mioyo yao, je, wanamwamini Mungu? Je, wanamwamini Mungu Mwenyewe yule wa kipekee? (La.) Kwa kuwa humwamini Mungu wa kipekee Mwenyewe, unamwamini nani? Kama unachoamini si Mungu Mwenyewe wa kipekee, kuna uwezekano unaamini katika sanamu, mtu maarufu, au Bodhisattva, kuwa unamwabudu Budha moyoni mwako. Zaidi ya hayo, kuna uwezekano unaamini katika mtu wa kawaida. Kwa muhtasari, kwa sababu ya aina tofautitofauti za imani za watu na mielekeo kwa Mungu, watu humweka Mungu wa utambuzi wao wenyewe katika nyoyo zao, wanamlazimishia Mungu fikira zao, wanaweka fikira na mielekeo yao kuhusu Mungu sambamba na Mungu Mwenyewe wa kipekee, na baadaye wanayadhihirisha ili yafanywe kuwa takatifu. Ina maana gani watu wakiwa na mielekeo hiyo isiyofaa kwa Mungu? Ina maana kuwa wamemkataa Mungu wa kweli Mwenyewe na kuabudu Mungu bandia, na ina maana kuwa wakati uleule wanapomwamini Mungu, wanamkataa Mungu, wanampinga, na kuwa wanakana uwepo wa Mungu wa kweli. Kama watu watazidi kushikilia imani za aina hiyo, matokeo yao yatakuwa gani? Kwa aina hiyo ya imani, je, wanaweza kufikia karibu na kutimiza matakwa ya Mungu? (La, hawawezi.) Kinyume cha hayo, kwa sababu ya dhana na fikira zao, watu watazidi kuwa mbali na njia ya Mungu, kwa kuwa njia wanayoifuata ni kinyume cha njia ambayo Mungu anawahitaji waifuata. Umekwisha kusikia hadithi ya “kwenda kusini kwa kuendesha gari la farasi kuelekea kaskazini”? Hii yaweza kuwa ni mfano wa kwenda kusini kwa kuendesha gari la farasi kuelekea kaskazini. Watu wakimwamini Mungu kwa njia hii ya kipumbavu, basi kadiri unavyojaribu kwa nguvu, ndivyo utakavyokuwa mbali zaidi na Mungu. Na kwa hiyo nakuonya hivi: Kabla ya kufunga safari, ni lazima kwanza ujue kama unaenda njia iliyo sawa. Lenga katika juhudi zako, kuwa na uhakika na kujiuliza, “Je, Mungu ninayemwamini ni Mtawala wa vitu vyote? Je, huyu Mungu ninayemwamini ni mtu tu wa kunipa riziki ya kiroho? Ni sanamu yangu? Je, huyu Mungu ninayemwamini anataka nini kutoka kwangu? Mungu huwa anakubali chochote ninachokifanya? Je, kila kitu ninachokifanya na kutafuta kinalingana na kazi ya kumjua Mungu? Je, kinalingana na mahitaji ya Mungu kwangu? Je, njia ninayoifuata inajulikana na kukubaliwa na Mungu? Je, Mungu anaridhishwa na imani yangu?” Aghalabu na mara kwa mara unafaa ujiulize haya maswali. Kama ungetaka kuutafuta ufahamu wa Mungu, basi lazima uwe na dhamiri safi na malengo wazi ndipo uweze kumridhisha Mungu.

Inawezekana kuwa, kutokana na ustahimilivu Wake, Mungu anaweza kukubali mielekeo hii

hasi ambayo Nimeizungumzia shingo upande? Mungu anaweza kuipongeza mielekeo ya watu hawa? (La.) Ni mahitaji yapi ya Mungu kwa wanadamu na wale ambao wanamfuata? Je, mnajua ni mwelekeo gani anaouhitaji kwa watu? Leo, nimezungumza mengi, nimezungumzia mengi kuhusu mada ya Mungu Mwenyewe, pamoja na matendo ya Mungu na kile Anacho na alichio. Sasa unajua ni kitu gani Mungu anatamani kupata kutoka kwa watu? Unajua ni kitu gani Mungu anataka kutoka kwako? Zungumzeni. Kama bado ufahamu wako kutokana na mazoea na matendo yako unakosa au ni wa juujuu sana, unaweza kusema kitu kuhusu ufahamu wako juu ya maneno haya. Una ufahamu kwa muhtasari? Ni kitu gani Mungu anahitaji kwa wanadamu? (Wakati wa huu ushirika mbalimbali, Mungu ametoa mkazo wa kututaka tumjue Mungu, tujue matendo Yake, tujue kuwa ni Yeye chanzo cha uhai kwa vitu vyote, tujue hadhi na utambulisho Wake.) Na ni nini matokeo ya mwisho Mungu anapohitaji watu wamjue? (Wajue kwamba Mungu ndiye Muumbaji, na kuwa watu ni viumbe walioumbwa.) Wanapopata ufahamu kama huu, ni mabadiliko yapi yanakuwepo katika mitazamo yao kwa Mungu, katika utekelezaji wao wa wajibu, au katika tabia zao? Umewahi kuwaza kuhusu hili? Inaweza kusemwa kuwa, baada ya kumjua Mungu na kumfahamu, wanakuwa watu wazuri? (Imani katika Mungu sio kwa ajili ya kuwa mtu mzuri. Bali, ni kutafuta kuwa kiumbe wa Mungu ambaye anafikia kiwango kilichotengwa, na kuwa mtu mwaminifu.) Kuna kitu kingine chochote? (Baada ya kumjua Mungu kweli na kwa usahihi, tunaweza kumtendea Mungu kama Mungu, tunajua kuwa Mungu daima ni Mungu, kuwa sisi ni viumbe walioumbwa, tunapaswa kumwabudu Mungu, na kusimama katika nafasi sahihi.) Vizuri sana! Hebu tusikie kutoka kwa wengine. (Tunamjua Mungu, na hatimaye tunaweza kuwa watu ambao wanamtii Mungu kweli, kumheshimu Mungu sana, na kuepuka maovu.) Huo ni ukweli.

3. Mwelekeo Ambao Mungu Anahitaji Mwanadamu Awe Nao Kwake

Kwa kweli, Mungu hana mahitaji sana kwa wanadamu—au angalau, hana mahitaji kama watu wanavyodhani. Ikiwa Mungu hangetamka maneno yoyote, ikiwa hangeonyesha tabia Yake au matendo yoyote, basi kumjua Mungu kungekuwa kugumu sana kwenu, kwa sababu watu wangelazimika kukisia nia ya Mungu na mapenzi Yake, kitu ambacho ni kigumu sana kwao. Lakini katika hatua ya mwisho ya Kazi Yake, Mungu amenena maneno mengi, kufanya kiwango kikubwa cha kazi, na kufanya mahitaji mengi kwa wanadamu. Katika maneno Yake, na kiwango kikubwa cha kazi Yake, amejulisha watu anachokipenda, anachokichukia, na wanafaa kuwa aina gani ya watu. Baada ya kuelewa vitu hivi, ndani ya nyoyo watu wanafaa kuwa na maelezo sahihi ya mahitaji ya Mungu, kwa kuwa hawamwamini Mungu wakiwa katika hali isiyo dhahiri na ya kinadharia, nahawamwabudu tena yule Mungu asiye yakini, au kumfuata Mungu katika ukosefu uyakini na udhahania na utupu; badala yake, watu wanaweza kusikia maneno ya Mungu, wanaweza kuelewa viwango vya mahitaji ya Mungu, na kuvifikia, na Mungu hutumia lugha ya

wanadamu kuwaambia watu yale yote wanafaa kujua na kulewa. Leo, kama watu bado hawamjui Mungu na kile Anachohitaji kutoka kwao; ikiwa hawajui kwa nini mtu anapaswa kumwamini Mungu, wala jinsi ya kumwamini ama kumtendea—basi kuna shida na hili. Sasa hivi tu kila mmoja wenu amezungumza kuhusu kipengele kimoja; mnafahamu kuhusu mambo fulani, yawe ni mambo mahususi au ya jumla—lakini Ningependa kuwaambia mahitaji ya Mungu ya kweli, kamili, na mahususi kwa wanadamu. Ni maneno machache tu, na rahisi sana. Yawezekana tayari mnayajua haya maneno. Mahitaji sahihi ya Mungu kwa wanadamu na wale ambao wanamfuata ni kama ifuatavyo. Mungu anahitaji mambo matano kutoka kwa wale wanaomfuata; imani ya kweli, ufuasi wenye uaminifu, utiifu kamili, ufahamu wa kweli na heshima za kutoka moyoni.

Katika mambo haya matano, Mungu anahitaji kuwa watu wasimshuku tena, wala kumfuata wakitumia fikira zao au mitazamo ikosayo uyakini na iliyo dhahania; Ni lazima wamfuata Mungu bila fikira au dhana zozote. Mungu anahitaji kuwa wote wanaomfuata wafanye hivyo kwa uaminifu, sio kwa shingo upande au bila kujizatiti. Mungu anapokupa mahitaji yoyote, au kukujaribu, kukuhukumu, kukushughulikia na kukupogoa, au kukuadhibu na kukuangamiza, unapaswa kuwa mtiifu kabisa Kwake. Hufai kuuliza kilichosababisha, au kuweka masharti, au hata uongee kuhusu sababu. Utiifu wako lazima uwe usio na shaka. Maarifa ya Mungu ni kipengele ambacho watu wengi wanakosea. Mara kwa mara wanamlazimishia Mungu misemo, matamshi, na maneno ambayo hayahusiani na Yeye, wakiamini kuwa haya maneno ndiyo ya kweli kuhusu kumfahamu Mungu. Kumbe hawajui kuwa hii misemo, ambayo inatoka kwa fikira za watu, ung'amuzi wao, na busara zao, havina uhusiano wowote na kiini cha Mungu. Na kwa hiyo, Ninataka kukwambia kuwa, katika ufahamu wa watu unaotamaniwa na Mungu, Mungu haulizi tu kwamba umtambue Mungu na maneno Yake, lakini kuwa ufahamu wako juu ya Mungu ni sahihi. Hata kama unaweza kusema sentensi moja tu, au una ufahamu mdogo tu, huu ufahamu mdogo ni sahihi na wa kweli, na unalingana na kiini cha Mungu Mwenyewe. Kwa kuwa Mungu hapendi sifa na wao kumtukuza Yeye kwa hali isiyo halisi na yenye nia mbaya. Zaidi ya hayo, Anachukia watu wanapomchukulia kama hewa. Anachukia ambapo, wakati wa majadiliano juu ya mada kuhusu Mungu, watu wanazungumza kimzaha, wakiongea kwa hiari bila ya kujali, wakiongea wapendavyo; zaidi ya hayo, anawachukia wale wanaojifanya wanamjua Mungu, na wanaringa kuhusu ufahamu wa Mungu, wakijadili mada kuhusu Mungu bila mipaka au kipimo. La mwisho Kati ya yale mahitaji matano lilikuwa ni kumheshimu Mungu kutoka moyoni. Hili ndilo hitaji kuu la Mungu kwa wale wote wanaomfuata. Wakati mtu ana ufahamu wa kweli na sahihi kumhusu Mungu, anaweza kumheshimu Mungu na kuepuka maovu. Heshima hii hutoka ndani ya moyo wake, ni ya hiari, na sio kwa sababu Mungu amemshurutisha. Mungu hataki utoe zawadi ya mwelekeo wowote wa kupendeza, au tabia, au mienendo ya nje Kwake; badala yake, anataka kwamba umheshimu na umwogope kutoka ndani ya moyo wako.

Heshima hii inaafikiwa kutokana na mabadiliko katika tabia ya maisha yako, kwa sababu una ufahamu juu ya Mungu, kwa sababu unaelewa matendo ya Mungu, kwa sababu ya uelewa wako wa kiini cha Mungu, na kwa sababu umetambua ukweli kuwa wewe ni mmoja wa viumbe wa Mungu. Na kwa hiyo, nia yangu ya kutumia neno “kutoka moyoni” kwa kurejelea heshima hapa ni kwamba wanadamu waelewe kuwa heshima ya watu kwa Mungu inapaswa kutoka ndani ya mioyo yao.

Sasa yafikirie hayo matakwa matano: kuna yeyote kati yenu anaweza kupata matatu ya kwanza? Ambapo Ninamaanisha uaminifu wa kweli, ufuasi wenye uaminifu, na utiifu kamili. Kuna wowote kati yenu wanaoweza mambo haya? Najua Nikisema yote matano, basi bila kuuliza hapatakuwa na hata mmoja kati yenu anayeweza—lakini nimeyapunguza hadi matatu. Tafakari kama umeyapata au la. Je, “uaminifu wa kweli” ni rahisi kuupata? (La, sio rahisi.) Sio rahisi, kwa kuwa mara nyingi watu humtilia Mungu mashaka. Na, je, “ufuasi wenye uaminifu”? Huu “uaminifu” una maana gani? (Sio kwa shingo upande ila kwa moyo wote.) Sio kwa shingo upande ila kwa moyo wote. Mmegonga ndipo! Kwa hiyo, je, mna uwezo wa kupata hili hitaji? Inabidi mjitahidi zaidi—siyo? Kwa sasa bado hamjapata hili hitaji. Kuhusu “utiifu kamili”—je, mmepata hilo? (Hapana.) Bado hamjapata hilo, pia. Mara nyingi nyinyi si watiifu na ni waasi, mara nyingi hamsikilizi, au kupenda kutii, au kutaka kusikia. Haya ndiyo mahitaji matatu ya msingi wanayopata watu baada ya kuingia katika maisha yao, na bado hamjayapata. Kwa hiyo, kwa wakati huu, mna uwezo mkubwa? Leo, baada ya kunisikia nikisema maneno haya, mna wasiwasi? (Ndiyo.) Ni sawa kuwa mna wasiwasi. Msiwe na wasiwasi Ninahisi wasiwasi kwa niaba yenu. Sitakwenda katika mahitaji hayo mengine mawili; bila shaka, hakuna anayeweza kuyafikia. Mna shauku. Kwa hivyo mmebaini malengo yenu? Malengo yapi, kuelekeza upande gani, mnapaswa kuyafuata, na kujitolea jitihada zenu? Mna lengo? Hebu niongee waziwazi: mnapofikia mahitaji haya matano, mtakuwa mmemridhisha Mungu. Kila mojawapo ni ishara, ishara ya watu wakiingia katika maisha wakiwa wamefikia ukomavu, na lengo la mwisho la hii. Hata kama Ningechukua moja kati ya mahitaji na kuongea kwa kina kulihusu na kinachohitajika, haiwezi kuwa rahisi kupata; ni lazima mpitie kiwango fulani cha matatizo na kufanya kiasi fulani cha juhudi. Na ni aina gani ya mawazo mnapaswa kuwa nayo? Yanapaswa kuwa sawa na yale ya mgonjwa wa saratani anayesubiri kwenda kwenye meza ya upasuaji. Na ni kwa nini Ninasema haya? Kama ungependa kumwamini Mungu, na kumpata Mungu na kupata ridhaa Yake, basi kama hutapitia katika kiasi fulani cha shida, au kufanya kiwango fulani cha juhudi, hutaweza kupata vitu hivi. Umesikia mahubiri mengi, lakini kuyasikia hakumaanishi kuwa haya mahubiri ni yako; ni lazima uyachukue na kuyageuza yawe kitu ambacho ni chako, ni lazima uyasimilishe maishani mwako, na kuyaleta katika uwepo wako, ukiyaruhusu maneno na mahubiri haya yakuongoze katika maisha yako, na kuleta dhamana na maana ya uhai katika maisha yako—na

hivyo basi itakuwa ni thamani kuwa uliyasikia maneno haya. Kama maneno haya Ninayoyanena hayaleti mabadiliko yoyote katika maisha yenu, au thamani yoyote katika uwepo wako, basi hakuna haja ya kuyasikiliza. Mnaelewa haya, ndiyo? Baada ya kuelewa haya, basi kilichobaki ni juu yenu wenyewe. Ni lazima mfanye kazi! Ni lazima muwe na bidii katika kila jambo! Msiwe huku na kule—wakati unapita upesi! Wengi wenu wamemwamini Mungu kwa zaidi ya miaka kumi. Fikiria nyuma kwa hii miaka kumi: Umenufaika kiasi gani? Na mmesalia na miongo mingapi ya haya maisha? Sio mirefu. Sahau kuhusu iwapo kazi ya Mungu inakusubiri, iwapo Amekuachia nafasi, iwapo Atafanya kazi ile ile tena; usizungumze kuhusu hili. Unaweza kurudisha nyuma miaka yako kumi iliyopita? Kwa kila siku inayopita, na kila hatua unayochukua, siku ambazo unazo hupunguzwa kwa siku moja. Muda haumsubiri mwanadamu yeyote! Utanufaika tu kutokana na imani kwa Mungu kama utaichukulia kama kitu kikubwa zaidi maishani mwako, muhimu zaidi kuliko chakula, mavazi, au kitu kingine chochote! Kama huwa unaamini tu unapokuwa na wakati, na huwezi kutoa umakini wako wote kwa imani yako, kama siku zote umetatizwa na vurugu, basi hutafaidi chochote. Unaelewa hili, ndio? Tutaishia hapa kwa leo. Tuonane wakati ujao! (Shukrani kwa Mungu!)

Februari 15, 2014

Kiambatisho: Kutazama Kuonekana kwa Mungu katika Hukumu na Kuadibu Kwake

Kama wale mamia ya mamilioni ya wengine wanaomfuata Bwana Yesu Kristo, tunafuata sheria na amri za Biblia, kufurahia neema tele ya Bwana Yesu Kristo, na kukusanyika pamoja, kuomba, kusifu, na kuhudumu kwa jina la Bwana Yesu Kristo—na haya yote sisi hufanya chini ya utunzaji na ulinzi wa Bwana. Mara nyingi, sisi huwa dhaifu, na mara nyingi sisi huwa pia wenye nguvu. Tunaamini kwamba matendo yetu yote yanaambatana na mafundisho ya Bwana. Na basi, ni dhahiri kwamba sisi pia tunajiamini kuwa kwenye njia ya kufanya mapenzi ya Baba aliye mbinguni. Tunatamani kurudi kwake Bwana Yesu, kushuka Kwake kwa utukufu, mwisho wa maisha yetu hapa duniani, kuonekana kwa ufalme, na kila kitu kama ilivyotabiriwa katika Kitabu cha Ufunuo: Bwana anafika, Analeta maafa, Anawazawadia walio wema na kuwaadhibu walio waovu, na Anawachukua wale wote wanaomfuata na kukaribisha kurudi Kwake juu kumlaki angani. Wakati wowote tunapowaza kuhusu haya, hatuwezi ila kujawa na hisia na kujawa na shukrani kwa kuwa tulizaliwa siku za mwisho na tuna bahati nzuri ya kushuhudia kuja kwake Bwana. Ingawa tumepitia mateso, tumepata badala yake “utukufu mkubwa na wa daima ambao unazidi kuwa mkuu kabisa.” Baraka gani hii! Hamu hii yote, na neema inayopewa na Bwana hutufanya kuingia kwenye maombi kwa kawaida, na hutufanya waangalifu zaidi katika

kukusanyika pamoja. Labda mwaka ujao, labda kesho, na tena, labda kwa muda mfupi zaidi kuliko binadamu anavyoweza kung'amua, Bwana ghafla atashuka, akionekana kati ya kundi la watu ambao wamekuwa wakimsubiri kwa faragha ya hamu. Tunaharakisha ili tuwe mbele ya wenzetu, hakuna anayetaka kubaki nyuma, yote kwa ajili ya kuwa kundi la kwanza la kutazama kuonekana kwa Bwana, ya kuwa miongoni mwa wale watakaonyakuliwa kwenda mbinguni. Tumetoa kila kitu, bila kujali gharama, kwa ajili ya kuwadia kwa siku hii, wengine wakiacha kazi zao, wengine wakiacha familia zao, wengine wakikana ndoa zao, na baadhi hata wakipeana akiba zao zote. Ni vitendo vya upendo usio na ubinafsi kweli! Uaminifu na utiifu kama huu bila shaka hata unashinda ule wa watakatifu wa nyakati za zamani! Kwa kuwa Bwana anampa neema yeyote yule ambaye Yeye anataka, na kumwonyesha huruma yeyote ambaye Yeye anataka, vitendo vyetu vya kujitolea na vya kutumia, tunaamini, vimetazamika machoni Pake kitambo. Kwa hivyo, pia, sala zetu za dhati zimefikia masikio Yake, na tunaamini kuwa Bwana atatulipa kwa ajili ya kujitolea kwetu. Aidha, Mungu alikuwa mwenye neema kwetu kabla hajauumba ulimwengu, na baraka na ahadi Ambazo ametupa hakuna anayeweza kuziondoa. Sote tunapanga kwa ajili ya siku za usoni, na bila shaka tumefanya kujitolea na kutumia kwetu kuwa vitu vya madai au raslimali ya kubadilishana kwa ajili ya kunyakuliwa kupatana na Bwana hewani. Kuongezea, bila kusita hata kidogo, sisi tumejiweka kwenye kiti cha enzi cha siku za baadaye, ili tutawale mataifa na watu wote kwa jumla, ama kutawala kama wafalme. Yote haya, sisi huchukulia kama jambo la lazima, kama kitu cha kutarajiwa.

Tunadharau wale wote walio kinyume na Bwana Yesu; wote wataishia kuangamizwa. Nani aliwaambia wasiamini kwamba Bwana Yesu ni Mwokozi? Bila shaka, kuna nyakati ambapo tunaiga Bwana Yesu katika kuwa na huruma kwa watu wa dunia, kwa kuwa hawaelewi, na ni sahihi kwamba tuwe wavumilivu na kuwasamehe. Kila kitu tufanyacho ni kwa mujibu wa maneno ya Biblia, kwani kila kitu ambacho hakifuatani na Biblia ni chenye kufuata imani tofauti na ni uzushi, Imani ya aina hii imekita mizizi katika akili ya kila mmoja wetu. Bwana wetu yumo katika Biblia, na tusipoondoka kwenye Biblia basi hatutaondoka kwa Bwana; tukitii kanuni hii, tutapata wokovu. Sisi huhimizana, kila akisaidia mwingine, na kila wakati tunapokusanyika pamoja ni matumaini yetu kwamba kila kitu tunachosema na kutenda kinaambatana na matakwa ya Bwana na kuwa kitabaliwa na Bwana. Licha ya uhasama mkali ulioko kwenye mazingira yetu, mioyo yetu imejaa furaha. Tunapowaza kuhusu baraka hizi tunazoweza kupata kwa urahisi, je, kuna kitu ambacho hatuwezi kukitenga kando? Je, kuna kitu ambacho hatuko tayari kuachana nacho? Yote haya hayapingwi, na haya yote yako chini ya macho angalifu ya Mungu. Sisi, walio wachache wa maskini ambao tumeinuliwa kutoka jaani, ni sawa tu na wafuasi wote wa Bwana Yesu wa kawaida tukiota kuhusu kunyakuliwa, na kubarikiwa, na kutawala mataifa yote. Upotovu wetu umeanikwa peupe machoni pa Mungu, na tamaa zetu na uchoyo zimehukumiwa

machoni pa Mungu. Hata hivyo, yote haya hutokea bila ajabu kabisa, na tena yenye mantiki sana, na hakuna hata mmoja kati yetu ambaye hushangaa kama hamu zetu ni za haki, sembuse yeyote kati yetu ambaye anashuku usahihi wa yote yale ambayo sisi hushikilia. Nani anayeweza kujua mapenzi ya Mungu? Njia hii hasa ni gani ambayo binadamu hutembelea, hatujui jinsi ya kutafuta, au kuchunguza, sembuse kujishughulisha nayo. Kwa maana sisi hujali tu kuhusu kama tutaweza kunyakuliwa, kama tunaweza kubarikiwa, kama kuna pahali tumetengewa katika ufalme wa mbinguni, na kama sisi tutaweza kupata mgawo wa maji ya mto wa uzima na matunda ya mti wa uzima. Je, si ni kwa ajili ya kupata vitu hivi ndiyo tunamwamini Bwana na kuwa wafuasi Wake? Dhambi zetu zimesamehewa, tumetubu dhambi zetu, tumekunywa kikombe cha mvinyo ambao ni mchungu, na tumeuweka msalaba migongoni mwetu. Nani anayeweza kusema kuwa Bwana hatafurahi kukubali gharama ambayo tumelipia? Nani anayeweza kusema kuwa hatujatayarisha mafuta yanayotosha? Hatungependa kuwa wale mabikira wapumbavu, ama mmoja wa wale ambao wameachwa. Aidha, tunaomba mara kwa mara, tukimwomba Bwana atuepushe kutokana na kudanganywa na Kristo wa uongo, kwa maana imeandikwa kwenye Biblia: “Basi iwapo mtu yeyote atawaambia, Tazameni, Kristo yuko huku, au yuko pale; msiamini hili. Kwa kuwa wataibuka makristo wasio wa kweli, na manabii wasio wa kweli, nao wataonyesha ishara kubwa na vioja; ili kwamba, ikiwezekana, watawadanganya walio wateule zaidi” (Mathayo 24:23-24). Sisi sote tumeweza mistari hii ya Biblia kwenye kumbukumbu, tunajua vyema sana, na tunaiona kama hazina ya thamani, kama hati ya muamana ambayo inaamua ikiwa tunaweza kuokolewa au kunyakuliwa ...

Kwa maelfu ya miaka, wanaoishi wamefariki, wakichukua tamaa zao na ndoto zao, lakini kuhusu iwapo wameenda kwa ufalme wa mbinguni, hakuna ajuaye hakika. Wafu wanarudi, wakiwa wamesahau hadithi zote zilizowahi kutokea wakati mmoja, na bado wanafuata mafundisho na njia za babu zetu. Na kwa njia hii, miaka inavyopita na siku zinavyosonga, hakuna anayejua iwapo Bwana Yesu, Mungu wetu, kwa kweli hukubali yote tunayoyafanya. Yote tuwezayo kufanya ni kutarajia tu kuwa na matokeo na kubashiri kuhusu yale yote ambayo yatakuja kutokea. Bado Mungu yu kimya siku zote, kamwe asionekane kwetu, kamwe asiseme nasi. Na kwa hivyo, kwa kufuata Biblia na kulingana na ishara tunahukumu mapenzi na tabia ya Mungu kwa hiari yetu. Sisi tumezoea kimya cha Mungu; tumekuwa na mazoea ya kupima usahihi na makosa ya mwenendo wetu kwa kutumia njia zetu wenyewe za mawazo: tumekuwa na mazoea ya kutegemea elimu yetu, dhana, na maadili yetu badala ya matakwa anazotutolea Mungu; tumekuwa na mazoea ya kufurahia neema ya Mungu; tumekuwa na mazoea ya Mungu kutoa msaada wakati sisi tunahitaji msaada huo; tumekuwa na mazoea ya kunyosha mikono yetu kwa Mungu ili tupate mambo yote, na kumuagiza Mungu; na pia tumekuwa na mazoea ya kufuata kanuni, kutotilia maanani jinsi Roho Mtakatifu hutuongoza; na, hata zaidi, tumekuwa na

mazoea ya siku ambazo sisi ni bwana zetu wenyewe. Tunamwamini Mungu wa namna hii, ambaye hatujawahi kukutana naye uso kwa uso. Maswali kama namna tabia Yake ilivyo, kile Anacho na Alichio, mfano Wake ulivyo, kama tutamjua ama hatutamjua wakati Atakaporudi, na kadhalika—haya yote hayana umuhimu. Jambo muhimu ni kuwa Yeye yumo mioyoni mwetu na kuwa tunamsubiri, na inatosha kuwa tunaweza kufikiria kwamba Yuko jinsi hii au jinsi ile. Tunathamini imani yetu, na kuthamini hali yetu ya kiroho. Tunaona kila kitu kikiwa kama samadi, na kukanyaga vitu vyote kwa nyayo zetu. Kwa sababu sisi ni wafuasi wa Bwana mwenye utukufu, bila kujali jinsi safari yetu ilivyo ndefu na ngumu, bila kujali shida na hatari zinazotukumba, hakuna kitu kitakachosimamisha nyayo zetu tunapomfuata Bwana. “Mto safi wa maji ya uhai, ung’ao kama kioo, uliondoka katika kiti cha Mungu cha enzi na cha Mwanakondoo. Na katika kila upande wa ule mto, ulikuwapo ule mti wa uhai unaozaa matunda ya jinsi kumi na mbili, na kuyatoa hayo matunda yake kila mwezi: na majani yake mti huu yalikuwa ya ajili ya kuyaponya mataifa. Na laana haitakuwepo tena: ila kiti cha Mungu cha enzi na cha Mwanakondoo kitakuwa ndani yake; na watumishi Wake watamhudumia: Na wao wataona uso Wake; nayo mapaji ya nyuso zao yatakuwa na jina Lake. Na hakutakuwa na usiku pale; wala hawahitaji mshumaa, wala mwanga wa jua; kwa sababu Bwana Mungu huwapa mwanga: na wao watatawala daima na milele” (Ufunuo 22:1-5). Kila wakati sisi hukariri maneno hayo, mioyo yetu hujawa na furaha isiyo na mipaka na maridhio, na machozi hutiririka kutoka machoni mwetu. Shukrani ni kwa Bwana kwa kutuchagua, shukrani ni kwa Bwana kwa neema Yake. Ametupa mara mia katika maisha haya, Yeye ametupa uzima wa milele kwa ulimwengu ujao. Kama Angetuomba tufe sasa, tungetii hiyo bila kusita hata kidogo. Ee Bwana! Tafadhali njoo hivi karibuni! Kwa kuwa sisi tunakutamani sana, na tumeacha kila kitu kwa ajili Yako, usikawie hata dakika moja, sekunde moja tena.

Mungu amenyamaza, na kamwe hawajawahi kujionyesha kwetu, ilhali kazi Yake haijawahi kusimama. Yeye huangalia dunia nzima, na huamuru vitu vyote, na kuona maneno yote na matendo yote ya mwanadamu. Yeye huendesha usimamizi Wake kwa hatua zilizopimwa na kulingana na mpango Wake kwa kimya, na bila madhara ya kutia shauku, ilhali nyayo Zake hukaribia, moja baada ya nyingine, daima hukaribia binadamu, na kiti Chake cha hukumu kimeenezwa katika ulimwengu kwa kasi ya umeme, na baada yake kiti Chake cha enzi mara moja hushuka kati yetu. Ni tukio la adhimu jinsi gani hilo, tukio hilo ni mandhari ya adhimu na yenye taadhima! Kama njiwa, na kama simba anayenguruma, Roho huja kati yetu. Yeye ni hekima, Yeye ni haki na uadhama, na Yeye huja kwa ukimya kati yetu, akiwa na mamlaka na akiwa amejawa na upendo na huruma. Hakuna mtu anayefahamu kuwasili Kwake, hakuna mtu anayekaribisha kuwasili kwake, na zaidi ya hayo, hakuna mwanadamu ambaye anajua chote ambacho yuko karibu kufanya. Maisha ya mwanadamu yanaendelea kama awali moyo wake

hauna tofauti, na siku zinapita kama kawaida. Mungu huishi kati yetu, mwanadamu kama watu wengine, kama mmoja wa wafuasi wasio na maana kabisa na kama muumini wa kawaida. Ana shughuli Zake Mwenyewe, malengo Yake mwenyewe, na zaidi ya hayo, Ana uungu usiomilikiwa na binadamu wa kawaida. Hakuna mtu ambaye ameona kuwepo kwa uungu Wake, na hakuna mtu ambaye ametambua tofauti ya kiini Chake na kile cha binadamu. Sisi huishi pamoja Naye, bila mipaka au kuogopa, kwa kuwa katika macho yetu, Yeye ni muumini asiye wa maana tu. Yeye huona matukio yetu yote, na fikra na mawazo yetu yote yanawekwa wazi mbele Yake. Hakuna mtu ambaye huwaza chochote kuhusu kazi Yake na isitoshe, hakuna aliye na shuku hata kidogo kuhusu kitambulisho Chake. Chote tunachofanya ni kuendelea na shughuli zetu, kana kwamba Yeye hahusiani nasi ...

Kwa bahati, Roho Mtakatifu huonyesha kifungu cha maneno “kupitia” Kwake, na hata ingawa inaonekana ni jambo lisilotarajiwa sana, tunalitambua hata hivyo kama tamko kutoka kwaa Mungu, na tunaukubali kwa urahisi kutoka kwa Mungu. Hii ni kwa sababu, bila kujali ni nani anayeonyesha maneno haya, ilimradi yanatoka kwa Roho Mtakatifu tunapaswa kuyakubali, na hatufai kuyakana. Tamko linalofuata linaweza kuja kupitia mimi, au wewe, ama kupitia yeye. Yeyote yule, yote ni neema ya Mungu. Ilhali bila kujali mtu huyo ni nani, hatufai kumwabudu mtu huyu, kwa kuwa bila kujali chochote, mtu huyu hawezi kuwa Mungu, wala hatuwezi kwa njia yoyote ile kumchagua mtu wa kawaida kama huyu kuwa ndiye Mungu wetu. Mungu wetu ni mkubwa na mwenye kuheshimika sana; mtu asiye na maana kama huyu anawezaje kusimama katika nafasi Yake? Zaidi ya hayo, tunamsubiri Mungu aje na kuturudisha kwa ufalme wa mbinguni, na kwa hivyo mwanadamu asiye na umuhimu hivyo anawezaje kuwa na sifa zinazostahili kufanya kazi ngumu na muhimu kama hiyo? Bwana akirudi tena, ni lazima iwe juu ya wingu jeupe, ambalo halaiki ya watu wanaweza kuliona. Huo utakuwa wa adhimu namna gani! Itawezekanaje kwamba Anaweza kujificha kwa siri kati ya kundi la watu wa kawaida?

Na bado ni huyu mtu wa kawaida, aliyefichika kati ya watu, ndiye anayefanya kazi hii mpya ya kutuokoa. Yeye hatupi maelezo yoyote, wala Hatuambii kwa nini amerudi, lakini Yeye anafanya tu kazi anayotarajia kufanya kwa hatua zilizopimwa, na kwa mujibu wa mpango Wake. Maneno Yake na matamshi Yake yanazidi kuja kwa wingi. Kuanzia kufariji, kuonya, kukumbusha, na kupeana onyo mpaka kukaripia na kufundisha nidhamu; kuanzia kutumia sauti ya upole na laini mpaka kutumia maneno makali na ya adhimu—lakini hakuna inayompa mwanadamu huruma na kumtia hofu. Kila kitu Anachosema kinatufikia kwetu na kulenga siri zilizofichwa ndani yetu, maneno Yake huchoma mioyo yetu, huchoma nafsi zetu, na hutuacha tukiwa tumejaa aibu isiyovumilika, tusijue pa kujificha. Tunaanza kutafakari iwapo Mungu Aliye katika roho ya huyu mtu kweli anatupenda, na nini hasa Anafanya. Labda tunaweza tu kunyakuliwa baada ya kuvumilia mateso haya? Vichwani mwetu tunafanya hesabu ... kuhusu

hatima inayokuja na kuhusu majaliwa yetu ya baadaye. Bado, kama awali, hakuna hata mmoja wetu anayeamini kwamba Mungu amechukua mwili tayari ili kutenda kazi kati yetu. Japokuwa Ametuandama kwa muda mrefu sana, ingawa tayari Yeye amesema maneno mengi uso kwa uso nasi, bado tunabaki bila hiari ya kumkubali mtu aliye wa kawaida kiasi hicho awe Mungu wa mustakabali wetu, na bado hatuna nia ya kumwaminisha mtu huyu asiye na maana udhibiti wa mustakabali na majaliwa yetu. Kutoka Kwake, tunafurahia ugavi usioisha wa maji ya uhai, na kupitia Kwake tunaishi uso kwa uso na Mungu. Lakini tunashukuru tu kwa neema ya Bwana Yesu aliye mbinguni, na hatujawahi kamwe kupa umakini hisia za huyu mtu wa kawaida mwenye kumilikiwa na uungu. Bado, kama awali Yeye kwa unyenyekevu, hufanya kazi Yake akiwa amefichwa ndani ya mwili, akipeana maonyesho a moyo Wake wa ndani zaidi, kana kwamba hafahamu kukataliwa Kwake na binadamu, kana kwamba yeye milele husamehe utoto na ujinga wa mwanadamu, na milele huvumilia mtazamo wa mwanadamu Kwake usioheshimu.

Pasipo sisi kujua, huyu mtu asiye muhimu ametuelekeza katika hatua moja baada ya nyingine ya kazi ya Mungu. Sisi hupitia majaribu tele, kuvumilia kurudi kusikohesabika, na tunajaribiwa na kifo. Tunapata kujua kuhusu tabia ya Mungu ya haki na uadhama, kufurahia, pia, upendo na huruma Zake, tunakuja kufahamu nguvu za Mungu ambazo ni kubwa na hekima Yake, tunashuhudia uzuri wa Mungu, na kutazama hamu Yake ya kumwokoza mwanadamu. Kwa maneno ya huyu mtu wa kawaida, tunakuja kujua tabia na kiini cha Mungu, kufahamu mapenzi ya Mungu, kujua asili ya mwanadamu na kiini cha mwanadamu, na tunapata kuona njia ya wokovu na ukamilifu. Maneno Yake hutufanya sisi “tufe,” na tena hutufanya “kuzaliwa upya”; maneno Yake hutufariji, na ilhali pia hutuacha tukiwa tumejawa na hatia na hisia ya kuwa wadeni; maneno Yake hutuletea furaha na amani, lakini pia maumivu makubwa sana. Wakati mwingine sisi ni kama wanakondoo wa kuchinjwa mikononi Mwake; wakati mwingine sisi ni kama kipenzi cha roho Yake na kufurahia upendo Wake wenye upole; wakati mwingine sisi ni kama adui Yake, na chini ya macho Yake tunageuzwa majivu na ghadhabu Yake. Sisi ni jamii ya wanadamu waliookolewa Naye, sisi ni funza machoni Pake, na sisi ni wanakondoo waliopotea ambao, usiku na mchana, Yeye hunuia kuwapata. Yeye ni mwenye huruma kwetu, hutudharau, Yeye hutuinua, Yeye hutufariji na kutuhimiza, Yeye hutuongoza, yeye hututia nuru, yeye huturudi na kutufundisha nidhamu, na Yeye hata hutulaani. Usiku na mchana, Yeye hakomi kamwe kuwa na wasiwasi nasi na hutulinda na kututunza usiku na mchana, Asiwache upande wetu kamwe, bali humwaga damu ya moyo Wake kwa ajili yetu na hulipia gharama yoyote kwa ajili yetu. Miongoni mwa matamshi ya mwili huu mdogo na wa kawaida wa nyama, tumefurahia ukamilifu wa Mungu na kuona hatima ambayo Mungu ametupa. Licha ya haya, majivuno bado yanazua rabsha mioyoni mwetu, na sisi bado hatuna nia ya kukubali kikamilifu mtu kama huyu kama Mungu wetu. Ingawa Yeye ametupa mana nyingi sana, nyingi sana ya kufurahia, hamna

kati ya haya ambalo linaweza kuchukua nafasi ya Bwana katika mioyo yetu. Tunaheshimu utambulisho maalum na hadhi ya huyu mwanadamu kwa kusita sana. Bora hafungui mdomo Wake kututaka tukiri kwamba Yeye ni Mungu, sisi kamwe hatuwezi kukata kauli wenyewe na kukiri Yeye ni Mungu ambaye yuko karibu kuja na ilhali amekuwa akifanya kazi kati yetu kwa muda mrefu sana.

Mungu huendelea na matamshi Yake, akitumia mbinu mbalimbali na mitazamo kutuonya kuhusu kile tunachofaa kufanya na wakati uo huo akipea moyo Wake sauti. Maneno Yake hubeba nguvu ya maisha, hutuonyesha njia tunayopasa kutembea, na yanatuwezesha kujua ukweli ni nini. Tunaanza kuvutiwa na maneno Yake, tunaanza kuzingatia sauti Yake na jinsi Anavyoongea, na bila hiari tunaanza kuvutiwa na hisia za ndani kabisa za mwanadamu huyu asiye wa ajabu. Yeye hutema damu ya moyo Wake kwa niaba yetu, hupoteza usingizi na hamu ya chakula kwa ajili yetu, analia kwa ajili yetu, anashusha pumzi kwa ajili yetu, anaugua magonjwa akigumia kwa ajili yetu, anadhalilishwa kwa ajili ya wokovu na hatima yetu, na uasi wetu na kufa ganzi kwetu kunatoa machozi na damu kutoka kwa moyo Wake. Njia hii ya kuwa na kumiliki si ya mtu wa kawaida, wala haiwezi kumilikiwa au kufikiwa na mtu yeyote aliyepotoka. Anaonyesha uvumilivu na subira isiyomilikiwa na mtu wa kawaida, na upendo Wake si kitu ambacho kiumbe chochote kimepewa. Hakuna mtu mbali na Yeye anayeweza kujua mawazo yetu yote, au kufahamu asili yetu na kiini chetu kwa dhahiri na ukamilifu, ama kuhukumu uasi na upotovu wa binadamu, ama kusema nasi na kufanya kazi kati yetu kama hivi kwa niaba ya Mungu aliye mbinguni. Hakuna mtu isipokuwa Yeye ambaye amepewa mamlaka, hekima, na heshima ya Mungu; tabia ya Mungu na kile Mungu Anacho na alichu yanatoka, kwa ukamilifu wao, ndani Yake. Hakuna mtu mbali na Yeye ambaye anaweza kutuonyesha njia na kutuletea mwangaza. Hakuna yeyote ila Yeye anayeweza kutufichulia siri ambazo Mungu hajatufunulia tangu uumbaji hadi leo. Hamna yeyote isipokuwa Yeye ambaye anaweza kutuokoa kutokana na utumwa wa Shetani na tabia yetu potovu. Yeye humwakilisha Mungu. Yeye huonyesha moyo wa ndani zaidi wa Mungu, ushawishi wa Mungu, na maneno ya hukumu ya Mungu kwa wanadamu wote. Ameanzisha enzi mpya, nyakati mpya, na kuleta mbingu na nchi mpya na kazi mpya, na ametuletea matumaini, akimaliza maisha ambayo tuliishi katika hali isiyo dhahiri, na kuwezesha nafsi yetu nzima kuona njia ya wokovu kwa udhahiri kamili. Ameshinda ubinadamu wetu wote, na kupata mioyo yetu. Tangu wakati huo na kuendelea, akili zetu zimepata ufahamu, na nafsi zetu huonekana kufufuka: Huyu mwanadamu wa kawaida asiye kuwa na umuhimu, ambaye huishi kati yetu na ambaye amekataliwa na sisi zamani—Je, huyu si ni Bwana Yesu, ambaye daima huwa kwa mawazo yetu, tukiwa tumeamka au kuota, na ambaye tunamtamani usiku na mchana? Ni Yeye! Ni Yeye kweli! Yeye ni Mungu wetu! Yeye ndiye ukweli, njia, na uzima! Yeye ametuwezesha kuishi tena na kuona nuru, na amekomesha mioyo

yetu kuhangaika. Tumerudi nyumbani mwa Mungu, tumerejea mbele ya kiti Chake cha enzi, tuko uso kwa uso pamoja na Yeye, tumeshuhudia uso Wake, na tumeona njia iliyo mbele. Wakati huu, mioyo yetu imeshindwa kabisa na Yeye; hatuna shaka kuhusu Yeye ni nani tena, hatupingi tena kazi Yake na neno Lake, na tunasujudu, mbele Yake. Hakuna tunachotaka zaidi yakufuata nyayo za Mungu maishani mwetu mwote, na kufanywa wakamilifu naye, na kulipa fadhila Yake, na kulipa upendo Wake kwetu, na kutii matayarisho na mipangilio Yake, na kushirikiana na kazi Yake, na kufanya kila kitu tunachoweza ili kukamilisha kile Anachotuaminia.

Kushindwa na Mungu ni kama mashindano ya kareti.

Kila neno la Mungu hugonga eneo letu moja la kufisha, likituwacha na uchungu na kujawa na hofu Yeye hufichua dhana zetu, mawazo yetu, na tabia zetu potovu. Kutoka kwa yale yote sisi husema na kutenda, hadi kwa kila wazo na fikra zetu, asili na kiini chetu kinafichuliwa katika maneno Yake, yakituweka katika hali ya hofu na kutetemeka na bila mahali pa kuficha aibu yetu. Mmoja baada ya mwingine, Anatueleza kuhusu matendo yetu yote, malengo yetu na nia, hata tabia potovu ambazo hatujawahi kugundua sisi wenyewe, na kutufanya tuhisi kwamba tumewekwa wazi katika dosari zetu mbaya na hata zaidi kushindwa kikamilifu. Yeye hutuhukumu kwa ajili ya upinzani wetu Kwake, hutuadibu kwa ajili ya kufuru kwetu na kumshutumu kwetu, na kutufanya tuhisi kwamba, machoni Pake, hatuna sifa hata moja inayoweza kutuokoa, kwamba sisi ndio Shetani anayeishi. Matumaini yetu yanavunjika, na hatuthubutu tena kumpa madai yoyote yasiyo na busara au kuendeleza matumaini yoyote ya Yeye, na hata ndoto zetu hupotelea mara moja. Huu ni ukweli ambao hakuna kati yetu anaweza kufikiria, na ambao hakuna yeyote kati yetu anayeweza kukubali. Katika muda mfupi, tunapoteza usawa wetu wa ndani, na hatujui jinsi ya kuendelea kwa njia iliyo mbele wala jinsi ya kuendelea katika imani zetu. Inaonekana kana kwamba imani yetu imerudi kama ilivyokuwa mwanzoni, na tena ya kana kwamba hatujawahi kukutana na Bwana Yesu au kupata kumjua. Kila kitu machoni petu hutujaza na mkanganyo, na kutufanya kuyumba kwa shaka. Tunasikitishwa, tunahuzunika, na ndani ya mioyo yetu kuna ghadhabu isiyoizulika na aibu. Tunajaribu kujieleza, kupata suluhisho, na, aidha, sisi huendelea kumsubiri Mwokozi Yesu, ili tuweze kujieleza kwa dhati Kwake. Ingawa kuna nyakati zingine ambazo sisi huonekana hatuyumbiyumbi kwa kutazamwa nje, tusio wenye kiburi wala wanyenyekevu, mioyoni mwetu tunateseka na hisia ya hasara kuliko ile tumewahi kuwa nayo. Ingawa wakati mwingine tunaweza kuonekana ni kama tuna utulivu kwa kutazamwa nje, akili zetu zinasokoteka kwa mateso kama bahari yenye dhoruba. Hukumu Yake na kuadibu Kwake zimechukua matumaini na ndoto zetu zote, kukomesha tamaa zetu kuu na kutuacha tusitake kuamini kuwa Yeye ndiye Mwokozi wetu na anayeweza kutuokoa. Hukumu Yake na kuadibu zimefungua ghuba kati yetu

na Yeye, ghuba kubwa kiasi kwamba hakuna aliye tayari hata kujaribu kuivuka. Hukumu na kuadibu Kwake ni mara ya kwanza ambapo sisi tumepitia pingamizi kubwa hivi, udhalilishaji kiasi kikubwa hivyo maishani mwetu. Hukumu na kuadibu Kwake kwa kweli zimetusakabisha kuthamini heshima ya Mungu na kutovumilia Kwake kosa la binadamu, ambazo tukilinganishwa nazo, sisi ni waovu sana, wachafu sana. Hukumu Yake na kuadibu zimetufanya sisi kutambua kwa mara ya kwanza jinsi ambavyo tuna kiburi na wenye majivuno, na jinsi ambavyo mwanadamu kamwe hataweza kulingana na Mungu, ama kuwa sawa na Mungu. Hukumu Yake na kuadibu Kwake zimetufanya tutumaini kutoishi tena katika tabia potovu hivi, kujiondoa asili na kiini hiki haraka iwezekanavyo, na kuwacha kuwa waovu na wa kuchukiwa na Yeye. Hukumu na kuadibu Kwake zimetufanya tufurahie kutii maneno Yake, na tusiasi matayarisho na mipangilio Yake tena. Hukumu na kuadibu Kwake kwa mara nyingine zimetuwezesha sisi tuwe na tamaa ya kuendelea kuwepo na zilituwezesha kufurahia kumkubali kama Mwokozi wetu.... Sisi tumetoka nje ya kazi ya ushindi, nje yaa kuzimu, tumetoka nje ya bonde la uvuli wa mauti.... Mwenyezi Mungu ametupata, kundi hili la watu! Ameshinda dhidi ya Shetani, na kuwashinda adui Zake wengi!

Sisi ni kundi la watu wa kawaida tu, waliomilikiwa na tabia potovu ya kishetani, wale waliochaguliwa na Mungu kabla ya enzi, na wale maskini ambao Mungu ameinua kutoka jaani. Kuna wakati tulipomkataa na kumshutumu Mungu, lakini sasa tumeshindwa na Yeye. Kutoka kwa Mungu tumepokea uzima, njia ya uzima wa milele. Licha ya mahali ambapo tunaweza kuwa duniani, licha ya mateso na dhiki tunazovumilia, hatuwezi kuwa mbali na wokovu wa Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa Yeye ndiye Muumba wetu, na ukombozi wetu pekee!

Upendo wa Mungu unaenea mbele kama maji ya chemichemi, na unapewa wewe, na mimi pia, na kwake, na kwa wale wote ambao wanatafuta ukweli kwa kweli na kungoja kuonekana kwa Mungu.

Kama vile tu mwezi hufuata jua kwa kubadilishana bila mwisho, vile vile ndivyo kazi ya Mungu haikomi kamwe, na inatekelezwa kwako, kwangu, kwake, na kwa wale wote ambao hufuata nyayo za Mungu na kukubali hukumu Yake na kuadibu Kwake.

Machi 23, 2010

Haya yaliandikwa na Mungu kama dibaji ya “Asili na Maendeleo ya Kanisa la Mwenyezi Mungu.”

Hitimisho

Ijapokuwa maneno haya yote si maonyesho ya Mungu, yanatosha kwa ajili ya watu kutimiza makusudi ya kumjua Mungu na badiliko katika tabia. Labda kuna wengine ambao

wanafikiri kuwa kwa sababu kazi ya Mungu katika bara ya China imekwisha, hili linathibitisha kuwa Amemaliza kutamka maneno yote ambayo Anapaswa kutamka, na kwamba hawezi kamwe kuwa na matamshi mapya kwani haya ndiyo maneno ambayo Mungu anaweza kunena. Zaidi ya hayo, kuna watu wanaoamini kuwa Neno Laonekana katika Mwili linajumuisha maonyesho yote ya Mungu katika Enzi ya Ufalme, na kwamba kupokea kitabu hiki ni sawa na kupokea kila kilicho cha Mungu, au kwamba kitabu hiki kitawaongoza wanadamu katika siku za usoni kama ilivyofanya Biblia. Ninaamini kwamba watu wanaoshikilia mitazamo hii si wachache, kwa kuwa watu daima wanapenda kumlazimishia Mungu mipaka. Ijapokuwa wote wanatangaza kuwa Mungu ni mwenye kudura na Amezunguka kila kitu, asili ya watu bado inawafanya kuwa wepesi wa kumwekea Mungu mipaka katika upeo fulani. Wakati uleule ambapo kila mtu anapata kumjua Mungu, vilevile wanamuasi na kumwekea mipaka.

Kazi ya Mungu katika Enzi ya Ufalme ndiyo tu imeanza. Matamshi yote ya Mungu katika kitabu hiki yalilengwa tu kwa wale waliomfuata wakati ule, na ni sehemu tu ya maonyesho ya Mungu katika kupata mwili Kwake kwa sasa, na hayawakilishi kila kitu cha Mungu. Zaidi ya hayo, haiwezi kusemwa kuwa inajumuisha kazi yote ambayo Mungu atafanya akiwa katika mwili huu wa sasa. Mungu atayalenga maneno Yake kwa watu wa makabila na asili tofauti, na Atawashinda wanadamu wote na kuitamatisha enzi ya zamani, hivyo basi Angekamilisha vipi baada ya kuonyesha sehemu ndogo kama hiyo ya maneno Yake? Ni kwamba tu kazi ya Mungu imegawanywa katika vipindi tofautitofauti vya wakati na hatua tofautitofauti. Anafanya kazi kulingana na mpango Wake na kuonyesha maneno Yake kulingana na hatua Zake. Ni vipi mwanadamu angeweza kuelewa kudura na busara za Mungu? Ukweli Ninaoufafanua hapa ni huu: Kile Mungu alichona anacho milele hakiishi wala hakina mipaka. Mungu ni chanzo cha uhai na vitu vyote. Mungu hawezi kueleweka na kiumbe yeyote aliyeumbwa. Mwishowe, ni lazima bado Nimkumbushe kila mtu: Msimwekee Mungu mipaka katika vitabu, maneno, au tena katika matamshi Yake yaliyopita. Kuna neno moja tu kwa sifa ya kazi ya Mungu—mpya. Hapendi kuchukua njia za zamani au kurudia kazi Yake, na zaidi ya hayo Hapendi watu kumwabudu kwa kumwekea mipaka katika upeo fulani. Hii ndiyo tabia ya Mungu.